# NENO
## BIBLIA TAKATIFU

Biblica® Toleo Wazi Neno: Bibilia Takatifu™
Hakimiliki © 1984, 1989, 2009, 2015 na Biblica, Inc.

Biblica® Open Kiswahili Contemporary Version™
Copyright © 1984, 1989, 2009, 2015 by Biblica, Inc.

"Biblica" is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

---

This work is made available under the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). To view a copy of this license, visit http:creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 or send a letter to Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® is a trademark registered by Biblica, Inc., and use of the Biblica® trademark requires the written permission of Biblica, Inc. Under the terms of the CC BY-SA license, you may copy and redistribute this unmodified work as long as you keep the Biblica® trademark intact. If you modify a copy or translate this work, thereby creating a derivative work, you must remove the Biblica® trademark. On the derivative work, you must indicate what changes you have made and attribute the work as follows: "The original work by Biblica, Inc. is available for free at www.biblica.com and open.bible."

Notice of copyright must appear on the title or copyright page of the work as follows:
Biblica® Toleo Wazi Neno: Bibilia Takatifu™
Hakimiliki © 1984, 1989, 2009, 2015 na Biblica, Inc.

Biblica® Open Kiswahili Contemporary Version™
Copyright © 1984, 1989, 2009, 2015 by Biblica, Inc.

"Biblica" is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.
You must also make your derivative work available under the same license (CC BY-SA).

If you would like to notify Biblica, Inc. regarding your translation of this work, please contact us at https:open.bible/contact-us.

# MAJINA NA TARATIBU YA VITABU VYOTE VYA

## AGANO LA KALE


Mwanzo . . . 9
Kutoka . . . 83
Mambo Ya Walawi . . . 147
Hesabu . . . 191
Kumbukumbu La Torati . . . 255
Yoshua . . . 311
Waamuzi . . . 347
Ruthu . . . 381
1 Samweli . . . 387
2 Samweli . . . 433
1 Wafalme . . . 475
2 Wafalme . . . 517
1 Mambo Ya Nyakati . . . 559
2 Mambo Ya Nyakati . . . 605
Ezra . . . 655
Nehemia . . . 671
Esta . . . 691
Ayubu . . . 701
Zaburi . . . 759
Mithali . . . 901
Mhubiri . . . 949
Wimbo Ulio Bora . . . 963
Isaya . . . 973
Yeremia . . . 1079
Maombolezo . . . 1175
Ezekieli . . . 1187
Danieli . . . 1263
Hosea . . . 1285
Yoeli . . . 1301
Amosi . . . 1307
Obadia . . . 1319
Yona . . . 1321
Mika . . . 1325
Nahumu . . . 1335
Habakuki . . . 1339
Sefania . . . 1345
Hagai . . . 1351
Zekaria . . . 1355
Malaki . . . 1369


## AGANO JIPYA


Mathayo . . . 1375
Marko . . . 1425
Luka . . . 1457
Yohana . . . 1511
Matendo Ya Mitume . . . 1551
Warumi . . . 1601
1 Wakorintho . . . 1623
2 Wakorintho . . . 1643
Wagalatia . . . 1657
Waefeso . . . 1665
Wafilipi . . . 1673
Wakolosai . . . 1679
1 Wathesalonike . . . 1685
2 Wathesalonike . . . 1689
1 Timotheo . . . 1693
2 Timotheo . . . 1699
Tito . . . 1703
Filemoni . . . 1707
Waebrania . . . 1709
Yakobo . . . 1727
1 Petro . . . 1733
2 Petro . . . 1739
1 Yohana . . . 1743
2 Yohana . . . 1749
3 Yohana . . . 1751
Yuda . . . 1753
Ufunuo . . . 1755

# DIBAJI

Hii ni tafsiri mpya ya Neno la Mungu katika lugha ya Kiswahili. Tafsiri hii ya *Neno: Biblia Takatifu* imetafsiriwa na Wakristo kutoka Tanzania na Kenya wa madhehebu mbalimbali. Imefanywa kwa ajili ya kutumiwa na Wakristo wa Kanisa la Mungu katika nchi zote ambako Kiswahili hutumika kama lugha ya mawasiliano.

Ziko tafsiri mbalimbali zilizotangulia kufanywa za Agano la Kale na Agano Jipya. Tunawashukuru sana wale waliofanya tafsiri hizi ambazo zimekuwa baraka kubwa kiroho. Basi kama ilivyo ada, lugha hukua. Kutokana na kukua huku, maneno mapya, misamiati, na hata matumizi hubadilika. Kadri mabadiliko yanavyotokea, watu wanajipata wakihitaji kupata ufahamu wa kiroho katika lugha itakayoeleweka kwa wepesi, bila kupoteza ile maana ya asili, usahihi, na uwazi ambavyo vitamwezesha msomaji kuelewa vyema yale anayoyasoma. Kutokana na hayo, imeonekana ni vyema kuwa na tafsiri hii ambayo itaeleweka kwa urahisi, na hatimaye kujenga umoja wa kiroho katika Kanisa la Mungu.

Tafsiri hii ya *Neno: Biblia Takatifu* ni toleo la kwanza ambalo limezingatia tafsiri za lugha za awali ili kupata maana zilizokusudiwa, na kuhakikisha kwamba kila neno limehakikiwa kwa ajili ya kuondoa utata wowote ambao ungeweza kujitokeza. Tafsiri hii ilipoanza kufanywa, ilipasa kutumia tafsiri mbalimbali za zamani au zilizotangulia ili kuweza kupata tafsiri ambayo itakidhi haja, njaa na kiu ya msomaji. Tulijitahidi kuepuka kila neno ambalo lingepunguza nguvu na mamlaka ya Neno la Mungu. Hivyo tulimwomba Roho Mtakatifu atupe neno au maneno yatakayobeba ujumbe alioukusudia. Kwa msingi huo, isidhaniwe kwamba kwenye tafsiri hii kuna mageuzi yoyote yaliyofanywa kwa Neno la Mungu. Jambo hilo kamwe halikufanyika.

Inatubidi tujue na tukumbuke kwamba Neno la Mungu halikuandikwa kwanza kwa Kiingereza wala Kiswahili. Roho Mtakatifu aliwavuvia watu watakatifu wa kale, yaani, Wayahudi na Wakristo, ili kuudhihirisha na kuutangaza ujumbe wa Mungu. Wayahudi waliandika ujumbe huo kwa Kiebrania na Kiaramu (iliyokuwa lugha ya biashara) na mahali pengine Kikaldayo katika Agano la Kale. Wakristo ambao idadi yao kubwa walikuwa watu wenye asili ya Kiyahudi waliandika Agano Jipya kwa Kiyunani, iliyokuwa lugha rasmi ya mawasiliano na biashara wakati huo. Kiaramu pia kimetumika sehemu mbalimbali.

Hivyo basi, watu wanaotafsiri Biblia katika lugha za kisasa kwanza huwa waangilifu sana ili kuhifadhi maana ya maneno ya asili ya lugha za awali, kisha hujitahidi kuandika tafsiri iliyo halisi. Haiwezekani kupata maana, mtiririko na ufahamu ikiwa ni tafsiri sisisi, yaani tafsiri ya neno kwa neno. Hivyo, watafsiri wa toleo hili wamezingatia umuhimu na kueleweka kwa neno husika. Wameepuka kutumia fafanusi na fasiri ambazo zingeadhiri maana za asili. Basi katika tafsiri hii, tumejitahidi kutumia maneno yanayoleta maana iliyokusudiwa na waandishi.

Watafsiri wamejaribu kuepuka mgongano wowote ambao ungeweza kujitokeza katika matumizi ya majina. Kwa mfano, Jina la Mungu katika Agano la Kale "Yehova," yaani, "Yhwh" kwa Kiebrania, limeandikwa Bwana, ikiwa na maana Yehova. Majina ya watu imebidi yafikiriwe na kuwekwa katika asili yake, kwa mfano Eva, Noa, Abrahamu, Yosefu, Mose, Maria, na kadhalika. Kwa hivyo majina ya watu na ya mahali imebidi yarekebishwe, jambo ambalo limeifanya kazi kuwa kubwa sana, kwani lilihitaji hadhari kubwa. Pale ambapo ilionekana neno halijulikani sana na hapatakuwa na budi kulitumia, neno hilo limewekwa kwenye rejeo chini ya ukurasa, au orodha ya maneno magumu mwishoni mwa kitabu, ili kumsaidia msomaji kupata maana.

Wakristo wote wanafahamu matumizi ya neno "Amin" au "Amen" kwa sababu yametumika kwa muda mrefu. Neno "Amin" linapotumika mwanzo wa usemi lina maana

“Ni kweli.” Neno “Amen” linapotumika mwisho wa usemi lina maana “Iwe hivyo.”

Toleo hili limezingatia kuweka vidokezo mbalimbali vya kumsaidia msomaji kutumia na kuweza kuelewa vizuri anaposoma Biblia. Baadhi ya vidokezo hivi ni: Utangulizi wa kila kitabu, kuweka vichwa vikuu na vidogo, kuweka maelezo ya neno au maneno ya Biblia ya asili chini ya ukurasa (rejeo), sura na aya zilizokolezwa, Itifaki, orodha ya maneno magumu, ramani na vielelezo, tabia za wanafunzi wa Yesu, uoanisho wa Injili, na utimilizo wa unabii wa Masiya katika Agano Jipya.

Tunawasihi mtuombee sisi tulioshirikiana katika kazi hii, ili Mungu atubariki sisi, na matunda ya kazi hii yawe mengi, tena yatakayompa Mungu utukufu. Maombi yetu ni kwamba Neno la Mungu litakuwa nuru kwa wengi, na litasababisha waijue kweli ya Mungu. Pia Neno la Mungu lilete umoja wa imani katika Kanisa la Mungu.

Nasi tunawaombea ninyi mtakaosoma Biblia hii, kwamba Roho Mtakatifu awape ufunuo wa kweli, na hili Neno liwe halisi katika maisha yenu ya kila siku. Mwisho, ombeni ili Roho Mtakatifu aiangazie mioyo ya wote wasomao na kutumia hili Neno, waweze kudumisha na kuendeleza utukufu Wake na kulijenga Kanisa la Yesu Kristo Bwana wetu.

Ni sisi,
Wenye kutafsiri.

# AGANO LA KALE

# MWANZO

*Siku Sita Za Uumbaji Na Sabato*

1 [a]Hapo mwanzo Mungu aliumba
mbingu na dunia. [2] [b]Wakati huu
dunia ilikuwa haina umbo, tena
ilikuwa tupu. Giza lilikuwa juu ya
uso wa vilindi vya maji, naye Roho
wa Mungu alikuwa ametulia juu ya
maji.

[3] [c]Mungu akasema, "Iwepo nuru,"
nayo nuru ikawepo. [4] [d]Mungu
akaona ya kuwa nuru ni njema,
ndipo Mungu akatenganisha nuru
na giza. [5] [e]Mungu akaiita nuru
"mchana," na giza akaliita "usiku."
Ikawa jioni, ikawa asubuhi, siku
ya kwanza.

[6] [f]Mungu akasema, "Iwepo nafasi
kati ya maji igawe maji na maji."
[7] [g]Kwa hiyo Mungu akafanya
nafasi, akatenganisha maji yaliyo
chini ya hiyo nafasi na maji yaliyo
juu yake. Ikawa hivyo. [8] [h]Mungu
akaiita hiyo nafasi "anga." Ikawa
jioni, ikawa asubuhi, siku ya pili.

[9] Mungu akasema, "Maji yaliyopo
chini ya anga na yakusanyike
mahali pamoja, pawepo na nchi
kavu." Ikawa hivyo. [10] [i]Mungu
akaiita nchi kavu "ardhi," nalo
lile kusanyiko la maji akaliita
"bahari." Mungu akaona kuwa ni
vyema.

[11] [j]Kisha Mungu akasema, "Ardhi
na itoe mimea: miche itoayo mbegu,
miti juu ya nchi itoayo matunda
yenye mbegu ndani yake, kila mmea
kulingana na aina zake mbalimbali."
Ikawa hivyo. [12] Ardhi ikachipua mimea:
Mimea itoayo mbegu kulingana na aina
zake, na miti itoayo matunda yenye
mbegu kulingana na aina zake. Mungu
akaona ya kuwa hili ni jema. [13] Ikawa
jioni, ikawa asubuhi, siku ya tatu.

[14] [k]Mungu akasema, "Iwepo mianga
kwenye nafasi ya anga ili
itenganishe usiku na mchana, nayo
iwe alama ya kutambulisha majira
mbalimbali, siku na miaka, [15] nayo
iwe mianga kwenye nafasi ya
anga ya kutia nuru juu ya dunia."
Ikawa hivyo. [16] [l]Mungu akafanya
mianga miwili mikubwa: mwanga
mkubwa utawale mchana, na
mwanga mdogo utawale usiku. Pia
Mungu akafanya nyota. [17] Mungu
akaiweka katika nafasi ya anga
iangaze dunia, [18] [m]itawale usiku
na mchana, na ikatenganishe nuru
na giza. Mungu akaona kuwa
hili ni jema. [19] Ikawa jioni, ikawa
asubuhi, siku ya nne.

[20] [n]Mungu akasema, "Kuwepo na

---

[a]**1:1** Za 89:11; 90:2; 96:5; 102:25; Mit 8:23; Isa 40:21; 42:5; 51:13; 41:4, 26; Yn 1:1-2; Mwa 2:3; 14:19; Neh 9:6; Ay 9:8; 37:18; Yer 10:12; 32:17; 51:15; 2Fal 19:15; Mdo 14:15; 7:24; Efe 3:9; Kol 1:16; Ebr 1:10; 3:4; 11:3; Ufu 4:11; 10:6

[b]**1:2** Isa 24:10; 27:10; 31:5; 32:14, 15; 34:11; 45:18; Yer 4:23; Mwa 8:2; Ay 7:12; 26:8; 33:4; 38:9; Za 36:6; 42:7; 104:6, 30; Mit 30:4

[c]**1:3** Za 33:6-9; 148:5; Ebr 11:3; 2Kor 4:6; 1Yn 5:7

[d]**1:4** Za 18:28; 105:8; 104:31; 119:68; Yer 31:35; Kut 10:21-23; Ay 26:10; 8:19; Isa 42:16; 45:7

[e]**1:5** Mwa 2:19, 23; Za 74:16

[f]**1:6** Isa 44:24; 2Pet 3:5; Za 24:2; 136:6

[g]**1:7** Mwa 7:11; Ay 26:10; 38:8-16; Za 68:33; 148:4; Mit 8:28

[h]**1:8** Ay 38:8-11; Za 33:7; 95:5; 104:6-9; Mit 8:29; Yer 5:22; 2Pet 3:5; Hag 2:6

[i]**1:10** Za 33:7; 90:2; 95:5; Ay 38:8

[j]**1:11** Za 65:9-13; 104:14; Mwa 2:9; Law 11:14, 19; 1Kor 15:38

[k]**1:14** Za 74:16; 136:7; 104:19; Yer 10:2; Mwa 8:22; Yer 31:35-36; 33:20, 25

[l]**1:16** Kum 17:3; Ay 38:33; 31:26; Yer 31:35; 43:13; Eze 8:16; Za 74:16; 104:19; 136:9; Yak 1:17; Kum 4:19

[m]**1:18** Yer 33:20

[n]**1:20** Za 146:6; Mwa 2:19

viumbe hai tele kwenye maji,
nao ndege waruke juu ya dunia
katika nafasi ya anga.” 21 [a]Kwa
hiyo Mungu akaumba viumbe
wakubwa wa baharini na kila
kiumbe hai kiendacho majini
kulingana na aina zake, na kila
ndege mwenye mabawa kulingana
na aina yake. Mungu akaona kuwa
hili ni jema. 22 [b]Mungu akavibariki,
akasema, “Zaeni mwongezeke,
mkayajaze maji ya bahari, nao
ndege waongezeke katika dunia.”
23 Ikawa jioni, ikawa asubuhi, siku
ya tano.

24 [c]Mungu akasema, “Ardhi na itoe
viumbe hai kulingana na aina
zake: wanyama wa kufugwa,
viumbe vitambaavyo ardhini
na wanyama pori, kila mnyama
kulingana na aina yake.” Ikawa
hivyo. 25 [d]Mungu akafanya
wanyama pori kulingana na aina
zake, wanyama wa kufugwa
kulingana na aina zake, na viumbe
vyote vitambaavyo juu ya ardhi
kulingana na aina zake. Mungu
akaona kuwa hili ni jema.

26 [e]Ndipo Mungu akasema, “Tufanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu, wakatawale juu ya samaki wa baharini na ndege wa angani, juu ya mifugo, juu ya dunia yote, na juu ya viumbe wote watambaao juu ya nchi.”

27 [f]Kwa hiyo Mungu akamuumba mtu
kwa mfano wake mwenyewe,
kwa mfano wa Mungu alimuumba;
mwanaume na mwanamke
aliwaumba.

28 [g]Mungu akawabariki na akawaambia, “Zaeni na mkaongezeke, mkaijaze tena dunia na kuitiisha. Mkatawale samaki wa baharini, ndege wa angani, na kila kiumbe hai kiendacho juu ya ardhi.”

29 [h]Kisha Mungu akasema,
“Nimewapa kila mche utoao mbegu
juu ya uso wa dunia yote, na kila mti
wenye matunda yenye mbegu ndani
yake. Vitakuwa chakula chenu. 30 [i]Nao
wanyama wote wa dunia, ndege wote
wa angani, na viumbe vyote viendavyo
juu ya ardhi: yaani kila kiumbe chenye
pumzi ya uhai, ninawapa kila mche
wa kijani kuwa chakula.” Ikawa hivyo.
31 [j]Mungu akaona vyote alivyoumba,
na tazama, ilikuwa vizuri sana. Ikawa
jioni, ikawa asubuhi, siku ya sita.

2 [k]Kwa hiyo mbingu na dunia zikakamilika, pamoja na vyote vilivyomo.

2 [l]Katika siku ya saba Mungu alikuwa
amekamilisha kazi aliyokuwa
akiifanya, hivyo siku ya saba
akapumzika kutoka kazi zake zote.
3 [m]Mungu akaibariki siku ya saba
akaifanya takatifu, kwa sababu
katika siku hiyo alipumzika kutoka
kazi zote za kuumba alizokuwa
amefanya.

---

[a]**1:21** Ay 3:8; 7:12; Za 74:13; 148:7; 104:25-26; Isa 27:1; Eze 32:2
[b]**1:22** Mwa 8:17; 47:27; 9:17, 19; Law 26:9; Eze 36:11
[c]**1:24** Mwa 2:19
[d]**1:25** Mwa 7:21-22; Yer 27:5
[e]**1:26** Mwa 5:3; 9:6; 9:2; Za 8:5-8; 8:8; 82:6; 89:6; Yak 3:9; 1Kor 11:7; 2Kor 4:4; Kol 1:15; 3:10; Mdo 17:28-29
[f]**1:27** Mwa 2:7; 5:1, 2; Za 103:14; 119:73; Mt 19:4; Mk 10:6; Gal 3:28; Kum 4:32
[g]**1:28** Mwa 6:1; 17:6; 33:5; Yos 24:3; Mdo 17:26; Za 8:6-8; 115:16; 113:9; 127:3, 5
[h]**1:29** Mwa 9:3; 1Tim 4:3; Kum 12:15; Za 104:14
[i]**1:30** Mwa 2:7; 7:22; Ay 38:41; Za 78:25; 104:14, 27; 111:5; 136:25; 145:15
[j]**1:31** Za 104:24; 136:5; Mhu 3:19; Yer 10:12; 1Tim 4:4
[k]**2:1** Kum 4:19; 17:3; 2Fal 17:16; 21:3; Za 104:2; Isa 44:24; 45:12; 48:13; 51:13
[l]**2:2** Kum 5:14; Ebr 4:4; Kut 20:11; 31:17; 34:21; Yn 5:17
[m]**2:3** Kut 16:23; 20:10; 23:12; 31:15; 35:2; Law 23:3; Ebr 4:11; Neh 9:14; Mwa 1:1; Za 95:11; Isa 58:13; Yer 17:22

*Adamu Na Eva*

4 [a]Haya ndiyo maelezo ya mbingu na
dunia wakati zilipoumbwa.

Bwana Mungu alipoziumba mbingu
na dunia, 5 [b]hapakuwepo na mche wa
shambani uliokuwa umejitokeza ardhini,
wala hapakuwepo na mmea wa shamba
uliokuwa umeota, kwa kuwa Bwana
Mungu alikuwa hajanyeshea mvua juu ya
nchi, na hapakuwepo mtu wa kuilima ardhi,
6 lakini umande ulitokeza kutoka ardhini
na kunyesha uso wote wa nchi: 7 [c]Bwana
Mungu alimuumba mtu kutoka mavumbi[d]
ya ardhi, akampulizia pumzi ya uhai puani
mwake, naye mtu akawa kiumbe hai.
8 [e]Basi Bwana Mungu alikuwa ameotesha
bustani upande wa mashariki, katika Edeni,
huko akamweka huyo mtu aliyemuumba.
9 [f]Bwana Mungu akafanya aina zote za miti
ziote kutoka ardhini, miti yenye kupendeza
macho na mizuri kwa chakula. Katikati ya
bustani ulikuwepo mti wa uzima na mti wa
kujua mema na mabaya.
10 [g]Mto wa kunyeshea bustani ulitiririka
toka Edeni, kuanzia hapa ukagawanyika
kuwa mito minne. 11 [h]Mto wa kwanza uliitwa
Pishoni, nao huzunguka nchi yote ya Havila
ambako kuna dhahabu. 12 [i](Dhahabu ya
nchi hiyo ni nzuri, bedola na vito shohamu
pia hupatikana huko.) 13 Jina la mto wa pili
ni Gihoni, ambao huzunguka nchi yote ya
Kushi. 14 [j]Jina la mto wa tatu ni Tigrisi,
unaopita mashariki ya Ashuru. Mto wa nne
ni Frati.
15 Bwana Mungu akamchukua huyo mtu,
akamweka kwenye Bustani ya Edeni ailime
na kuitunza. 16 [k]Bwana Mungu akamwagiza
huyo mtu, akamwambia, “Uko huru kula
matunda ya mti wowote katika bustani,
17 [l]lakini kamwe usile matunda ya mti
wa kujua mema na mabaya, kwa maana
siku utakapokula matunda yake, hakika
utakufa.”
18 [m]Bwana Mungu akasema, “Si vyema
huyu mtu awe peke yake. Nitamfanyia
msaidizi wa kumfaa.”
19 [n]Basi Bwana Mungu alikuwa
amefanyiza kutoka ardhi wanyama wote wa
porini na ndege wote wa angani. Akawaleta
kwa huyu mtu aone atawaitaje, nalo jina
lolote alilokiita kila kiumbe hai, likawa
ndilo jina lake. 20 [o]Hivyo Adamu akawapa
majina wanyama wote wa kufugwa, ndege
wa angani, na wanyama wote wa porini.

Lakini kwa Adamu hakupatikana
msaidizi wa kumfaa. 21 [p]Hivyo Bwana
Mungu akamfanya Adamu kulala usingizi
mzito, naye alipokuwa amelala akachukua
moja ya mbavu zake, akapafunika mahali
pale kwa nyama. 22 [q]Kisha Bwana Mungu
akamfanya mwanamke kutoka kwenye
ule ubavu aliouchukua kutoka kwa huyo
mwanaume, akamleta huyo mwanamke
kwa huyo mwanaume.
23 [r]Huyo mwanaume akasema,

“Huyu sasa ni mfupa wa mifupa
yangu
na nyama ya nyama yangu,

[a]**2:4** Mwa 5:1; 6:9; 1:1; 10:1; 11:10; 27:25; Ay 38:8-11
[b]**2:5** Mwa 1:11; Ay 38:28; Za 65:9-10; Yer 10:13
[c]**2:7** Isa 29:16; 43:1, 21; 44:2; Mwa 1:27; 3:19; 18:27; 5:23; 4:2; Ay 4:19; 10:9; 17:16; 34:15; Za 103:14; 90:3; Mhu 3:20; 12:7
[d]7 Neno la Kiebrania la mavumbi ya ardhi ndilo kiini cha jina Adamu.
[e]**2:8** Mwa 3:23-24; 4:16; 13:10; Isa 51:3; Eze 28:13; 36:35; 31:9, 16; Yoe 2:3
[f]**2:9** Eze 31:8; 47:12; Mit 3:18; 11:30; Ufu 2:7; Mwa 3:22, 24
[g]**2:10** Hes 24:6; Eze 47:5; Za 46:4
[h]**2:11** Mwa 10:7; 25:18
[i]**2:12** Hes 11:7
[j]**2:14** Mwa 15:18; 41:1; 31:21; Dan 10:4; Kut 23:31; Hes 22:5; Ufu 9:14; 1Fal 4:21; 2Sam 8:3; Kum 11:24; 2Fal 23:29; 24:7; 1Nya 5:9; 18:3; 2Nya 35:20; Yer 13:4; 42:6; 51:63
[k]**2:16** Mwa 3:1-2
[l]**2:17** Mwa 3:11, 17; 9:29; Yer 42:16; Kum 30:15, 19; Eze 3:18; Rum 5:13; 6:23
[m]**2:18** Mit 11:31; 1Kor 11:9; 1Tim 2:13
[n]**2:19** Za 8:7; Mwa 1:5, 20, 24
[o]**2:20** Mwa 3:20; 4:1
[p]**2:21** Mwa 15:12; 1Sam 26:12; Ay 33:15
[q]**2:22** 1Kor 11:8-9, 12; 1Tim 2:12
[r]**2:23** Mwa 29:14; Efe 5:28-30; 1Kor 11:8

ataitwa 'mwanamke,'[a]
kwa kuwa alitolewa katika
mwanaume."

24 [b]Kwa sababu hii mwanaume atamwacha
baba yake na mama yake na kuambatana
na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja.
25 [c]Adamu na mkewe wote wawili
walikuwa uchi, wala hawakuona aibu.

*Kuanguka Kwa Mwanadamu*

3 [d]Basi nyoka alikuwa mwerevu kuliko
wanyama wote wa porini ambao BWANA
Mungu aliwafanya. Nyoka akamwambia
mwanamke, "Ati kweli Mungu alisema,
'Kamwe msile matunda ya mti wowote wa
bustanini'?"
2 [e]Mwanamke akamjibu nyoka,
"Tunaweza kula matunda ya miti iliyoko
bustanini, 3 lakini Mungu alisema, 'Kamwe
msile tunda la mti ulio katikati ya bustani,
wala kuugusa, la sivyo mtakufa.' "
4 [f]Lakini nyoka akamwambia mwanamke,
"Hakika hamtakufa. 5 [g]Kwa maana Mungu
anajua ya kuwa wakati mtakapoyala, macho
yenu yatafumbuliwa, nanyi mtakuwa kama
Mungu, mkijua mema na mabaya."
6 [h]Mwanamke alipoona ya kuwa tunda
la mti huo lilikuwa zuri kwa chakula na la
kupendeza macho, tena linatamanika kwa
kujipatia hekima, basi akachuma katika
matunda yake, akala, pia akampa mumewe,
aliyekuwa pamoja naye, naye akala. 7 [i]Ndipo
macho yao wote wawili yakafumbuliwa,
wakajiona kwamba walikuwa uchi; hivyo
wakashona majani ya mtini, wakajifunika.
8 [j]Ndipo yule mwanaume na mkewe,
waliposikia sauti ya BWANA Mungu
alipokuwa akitembea bustanini jioni,
wakajificha kutoka mbele za BWANA Mungu
katikati ya miti ya bustani. 9 [k]Lakini BWANA
Mungu akamwita Adamu, "Uko wapi?"
10 [l]Naye akajibu, "Nilikusikia katika
bustani nikaogopa kwa sababu nilikuwa
uchi, hivyo nikajificha."
11 [m]Mungu akamuuliza, "Ni nani
aliyekuambia ya kuwa ulikuwa uchi? Je,
umekula matunda ya mti niliokuamuru
usile?"
12 [n]Adamu akasema, "Huyu mwanamke
uliyenipa awe pamoja nami alinipa sehemu
ya tunda kutoka kwenye huo mti, nami
nikala."
13 [o]Ndipo BWANA Mungu akamuuliza
mwanamke, "Ni nini hili ambalo
umelifanya?" Mwanamke akajibu, "Nyoka
alinidanganya, nami nikala."
14 [p]Hivyo BWANA Mungu akamwambia
nyoka, "Kwa kuwa umefanya hili,

"Umelaaniwa kuliko wanyama wote
wa kufugwa na wa porini!
Utatambaa kwa tumbo lako
na kula mavumbi
siku zote za maisha yako.
15 [q]Nami nitaweka uadui
kati yako na huyo mwanamke,
na kati ya uzao wako na wake,
yeye atakuponda kichwa,
nawe utamuuma kisigino."

---

[a]23 Jina la Kiebrania la mwanamke linafanana na lile la mwanaume.
[b]**2:24** Mal 2:15; Mt 19:5; Mk 10:7-8; Efe 5:31; 1Kor 6:16
[c]**2:25** Mwa 3:7, 10-11; Isa 47:3; Mao 1:8
[d]**3:1** Ay 1:7; 2:2; 2Kor 11:3; Ufu 12:9; 20:2; Mwa 2:17
[e]**3:2** Mwa 2:16-17
[f]**3:4** Yn 8:44; 2Kor 11:3
[g]**3:5** Mwa 1:26; 14:18-19; Za 7:8; Isa 14:14; Eze 28:2
[h]**3:6** Yak 1:14-15; 1Yn 2:16; Hes 30:7-8; Yer 44:15, 19, 24; 2Kor 11:3; 1Tim 2:14
[i]**3:7** Mwa 2:25
[j]**3:8** Law 26:12; Kum 23:14; Ay 13:16; 23:7; 34:22-23; Isa 29:15; Za 139:7-12; Yer 16:17; 23:24; 49:10; Ufu 6:15-16
[k]**3:9** Mwa 4:9; 16:8; 18:9; 1Fal 19:9-13
[l]**3:10** Kut 19:16; 20:18; Kum 5:5; Mwa 2:25; 1Sam 12:18
[m]**3:11** Mwa 2:17, 25
[n]**3:12** Mwa 2:22
[o]**3:13** Rum 7:11; 2Kor 11:3; 1Tim 2:14
[p]**3:14** Za 72:9; Mik 7:17; Kum 28:15-20; Isa 49:23; 65:25
[q]**3:15** Yn 8:44; 1Yn 3:8; Mdo 13:10; Mwa 16:11; Amu 13:5; Ebr 2:14; Isa 7:14; 8:3; 9:6; Mt 1:23; Lk 1:31; Gal 4:4; Ufu 12:17; Rum 16:20

16 [a]Kwa mwanamke akasema,

“Nitakuzidishia sana utungu wakati
wa kuzaa kwako;
kwa utungu utazaa watoto.
Tamaa yako itakuwa kwa mumeo
naye atakutawala.”

17 [b]Kwa Adamu akasema, “Kwa sababu
umemsikiliza mke wako na ukala kutoka
kwenye mti niliokuamuru, ‘Msile tunda
lake,’

“Ardhi imelaaniwa kwa sababu yako,
kwa kazi ngumu utakula chakula
kitokacho humo
siku zote za maisha yako.
18 [c]Itazaa miiba na mibaruti kwa ajili
yako,
nawe utakula mimea ya shambani.
19 [d]Kwa jasho la uso wako
utakula chakula chako
hadi utakaporudi ardhini,
kwa kuwa ulitwaliwa kutoka
humo,
kwa kuwa wewe u mavumbi
na mavumbini wewe utarudi.”

20 [e]Adamu akamwita mkewe Eva, kwa
kuwa atakuwa mama wa wote walio hai.
21 Bwana Mungu akawatengenezea
Adamu na mkewe mavazi ya ngozi,
akawavika. 22 [f]Kisha Bwana Mungu
akasema, “Sasa mtu huyu amekuwa kama
mmoja wetu, kwa kujua mema na mabaya.
Sharti asiruhusiwe kunyoosha mkono wake
na kuchuma pia kutoka mti wa uzima akala,
naye akaishi milele.” 23 [g]Hivyo Bwana
Mungu akamfukuzia mbali kutoka Bustani
ya Edeni, akalime ardhi ambamo alitolewa.
24 [h]Baada ya kumfukuzia mbali Adamu,
Mungu akaweka makerubi mashariki ya
Bustani ya Edeni, pamoja na upanga wa
moto ukimulika huku na huko kulinda njia
ya kuuendea mti wa uzima.

### *Kaini Na Abeli*

4 [i]Adamu akakutana kimwili na mkewe
Eva, naye akapata mimba, akamzaa
Kaini. Eva akasema, “Kwa msaada wa
Bwana nimemzaa mwanaume.” 2 [j]Baadaye
akamzaa Abeli ndugu yake.
Basi Abeli akawa mfugaji, na Kaini akawa
mkulima. 3 [k]Baada ya muda Kaini akaleta
baadhi ya mazao ya shamba kama sadaka
kwa Bwana. 4 [l]Lakini Abeli akaleta fungu
nono kutoka baadhi ya wazaliwa wa kwanza
wa mifugo yake. Bwana akamkubali Abeli
pamoja na sadaka yake, 5 lakini Mungu
hakumkubali Kaini pamoja na sadaka yake.
Kwa hiyo Kaini akakasirika sana, uso wake
ukawa na huzuni.
6 Kisha Bwana akamwambia Kaini,
“Kwa nini umekasirika? Kwa nini uso
wako una huzuni? 7 [m]Ukifanya lililo sawa,
je, hutakubalika? Lakini usipofanya lililo
sawa, dhambi inakuvizia mlangoni mwako,
inakutamani wewe, lakini inakupasa
uishinde.”
8 [n]Basi Kaini akamwambia ndugu yake
Abeli, “Twende shambani.” Walipokuwa
shambani, Kaini akamshambulia Abeli
ndugu yake, akamuua.
9 [o]Kisha Bwana akamuuliza Kaini,
“Ndugu yako Abeli yuko wapi?”

---

[a]**3:16** Za 48:5-6; Isa 13:8; 21:3; 26:17; Yer 4:31; 6:24; Mik 4:9; 1Kor 11:3; Efe 5:22; 1Tim 2:15
[b]**3:17** Mwa 2:17; 5:29; 6:13; 8:21; 47:9; 29:32; 31:42; Hes 35:33; Za 66:11; 106:39; 127:2; Isa 24:5; Rum 8:20-22; Isa 54:9; Kut 3:7; Mhu 1:13; 2:23; Ay 5:7; 14:1; Yer 20:18
[c]**3:18** Za 104:14; Ay 31:40; Isa 5:6; Ebr 6:8
[d]**3:19** Mwa 2:7; 14:18; Kum 8:3, 9; 23:4; Rum 1:6; 2:14; 2The 3:10; Ay 7:21; Ebr 9:27; Za 146:4; 104:23; Rut 1:6; 2:14; 1Kor 15:47
[e]**3:20** Mwa 2:20; 2Kor 11:3; 1Tim 2:13
[f]**3:22** Mwa 2:9; 1:26; Ufu 2:7
[g]**3:23** Mwa 2:7-8
[h]**3:24** Kut 25:18-22; 1Sam 4:4; 2Sam 6:2; 22:11; 1Fal 6:27; 8:6; 2Fal 19:15; 2Nya 5:8; Za 18:10; 104:4; Isa 27:1; 37:16; Eze 10:1; Mwa 2:9; Ay 40:19
[i]**4:1** Mwa 2:20; Ebr 11:4; 1Yn 3:12; Yud 11
[j]**4:2** Mt 23:35; Lk 11:51; Ebr 11:4; 12:24; Mwa 2:7
[k]**4:3** Law 2:1-2; Isa 43:23; Yer 41:5; Hes 18:12
[l]**4:4** Law 3:16; 2Nya 29:35; Kut 13:2, 12; Kum 15:19; Ebr 11:4
[m]**4:7** Mwa 44:16; Hes 32:23; Isa 59:12; Ay 11:15; 22:27; Za 27:3; 46:2; Rum 6:16
[n]**4:8** Mt 23:35; Lk 11:51; 1Yn 3:12; Yud 11
[o]**4:9** Mwa 3:9; Yn 8:44

Akamjibu, “Sijui, je, mimi ni mlinzi wa
ndugu yangu?”
10 [a]BWANA akasema, “Umefanya nini?
Sikiliza! Damu ya ndugu yako inanililia
mimi kutoka ardhini. 11 [b]Sasa umelaaniwa
na umehamishwa kutoka ardhi, ambayo
imefungua kinywa chake na kupokea damu
ya ndugu yako kutoka mkononi mwako.
12 [c]Utakapoilima ardhi, haitakupa tena
mazao yake. Utakuwa mtu wa kutangatanga
duniani asiye na utulivu.”
13 Kaini akamwambia BWANA, “Adhabu
yangu ni zaidi ya niwezavyo kustahimili.
14 [d]Leo unanifukuza kutoka nchi, nami
nitafichwa mbali na uwepo wako. Nitakuwa
mtu wa kutangatanga asiyetulia duniani na
yeyote anionaye ataniua.”
15 [e]Lakini BWANA akamwambia, “La
sivyo, ikiwa mtu yeyote atamuua Kaini
atalipizwa kisasi mara saba zaidi.” Kisha
BWANA akamwekea Kaini alama ili mtu
yeyote ambaye angemwona asimuue.
16 [f]Kwa hiyo Kaini akaondoka mbele za
BWANA akaenda kuishi katika nchi ya Nodi,
iliyoko mashariki ya Edeni.
17 [g]Kaini akakutana kimwili na mkewe,
naye akapata mimba na akamzaa Enoki.
Wakati huo Kaini alikuwa anajenga mji,
akauita Enoki jina la mtoto wake. 18 Enoki
akamzaa Iradi, Iradi akamzaa Mehuyaeli,
Mehuyaeli akamzaa Methushaeli, na
Methushaeli akamzaa Lameki.
19 [h]Lameki alioa wanawake wawili,
mmoja aliitwa Ada, na mwingine Sila.
20 Ada akamzaa Yabali ambaye ni baba wa
wale walioishi katika mahema na kufuga
wanyama. 21 [i]Kaka yake aliitwa Yubali,
aliyekuwa baba wa wote wapigao zeze
na filimbi. 22 [j]Pia Sila alikuwa na mtoto
wa kiume aliyeitwa Tubali-Kaini ambaye
alifua vifaa vya aina mbalimbali vya
shaba na chuma. Naama alikuwa dada wa
Tubali-Kaini.
23 [k]Lameki akawaambia wake zake,

“Ada na Sila nisikilizeni mimi;
wake wa Lameki sikieni maneno
yangu.
Nimemuua mtu kwa kunijeruhi,
kijana mdogo kwa kuniumiza.
24 [l]Kama Kaini atalipizwa kisasi mara
saba,
basi Lameki itakuwa mara sabini
na saba.”

25 [m]Adamu akakutana kimwili na mke
wake tena, akamzaa mwana, akamwita
Sethi, akisema, “Mungu amenijalia mwana
mwingine badala ya Abeli, kwa kuwa Kaini
alimuua.” 26 [n]Naye Sethi akamzaa mwana,
akamwita Enoshi.

Wakati huo watu wakaanza kuliitia jina
la BWANA.

*Kutoka Adamu Hadi Noa*

**(1 Nyakati 1:1-4)**

5 [o]Hii ni orodha iliyoandikwa ya vizazi
vya Adamu.

Wakati Mungu alipomuumba
Adamu, alimfanya kwa sura ya Mungu.
2 [p]Aliwaumba mwanaume na mwanamke,

---

[a]**4:10** Mwa 9:5; 37:20, 26; Kut 21:12; Hes 35:33; Kum 21:7-9; 2Sam 4:11; Ay 16:18; 24:2; 31:38; Za 9:12; 106:38; Ebr 12:24; Ufu 6:9-10
[b]**4:11** Kum 11:28; 2Fal 2:24
[c]**4:12** Kum 28:15-24; Za 37:25; 59:15; 109:10
[d]**4:14** 2Fal 17:18; Za 51:11; 139:7-12; Yer 7:15; 52:3; Kum 28:64-67; Mwa 9:6; Kut 21:12-14; Law 24:17; Hes 35:19-21, 27; 1Fal 2:32; 2Fal 11:16
[e]**4:15** Eze 9:4, 6; Kut 21:20; Law 26:21; Za 79:12
[f]**4:16** Yud 11; Mwa 2:8
[g]**4:17** Za 55:9; 49:11
[h]**4:19** Mwa 2:9; 29:28; Kum 21:15; Rut 4:11; 1Sam 1:2
[i]**4:21** Mwa 31:27; Kut 15:20; 1Sam 16:16; 1Nya 25:3; Za 33:2; 43:4; 150:4; Isa 16:11; Dan 3:5; Ay 21:12; 30:31
[j]**4:22** Kut 35:35; 1Sam 13:19; 2Fal 24:14
[k]**4:23** Mwa 9:6-9; Kut 20:13; 21:12; 23:7; Law 19:18; 24:17; Kum 27:24
[l]**4:24** Kum 32:35; 2Fal 9:7; Za 18:47; Isa 35:4; Yer 51:56; Mt 18:22; Nah 1:2
[m]**4:25** Mwa 5:3; 1Nya 1:1
[n]**4:26** Mwa 5:3; 12:8; 13:4; 21:33; 22:9; 26:25; 33:20; Lk 3:38; Kut 17:15; Sef 3:9; 1Fal 18:24; Za 116:17; Yoe 2:32; Mdo 2:21
[o]**5:1** Mwa 1:27; 2:4; 1Nya 1:1; Kol 3:10; Efe 4:24
[p]**5:2** Mwa 1:27-28; Mt 19:4; Mk 10:6; Gal 3:28

akawabariki. Walipokwisha kuumbwa,
akawaita “mwanadamu.”
3 [a]Adamu alipokuwa ameishi miaka 130,
alikuwa na mwana aliyekuwa na sura yake,
mwenye kufanana naye. Akamwita Sethi.
4 Baada ya Sethi kuzaliwa, Adamu aliishi
miaka 800, akawa na watoto wengine wa
kiume na wa kike. 5 [b]Adamu aliishi jumla
ya miaka 930, ndipo akafa.
6 [c]Sethi alipokuwa ameishi miaka 105,
akamzaa Enoshi. 7 Baada ya kumzaa Enoshi,
Sethi aliishi miaka 807, akawa na watoto
wengine wa kiume na wa kike. 8 Sethi
aliishi jumla ya miaka 912, ndipo akafa.
9 [d]Enoshi alipokuwa ameishi miaka tisini,
akamzaa Kenani. 10 Baada ya kumzaa
Kenani, Enoshi aliishi miaka 815, naye
alikuwa na watoto wengine wa kiume na
wa kike. 11 Enoshi aliishi jumla ya miaka
905, ndipo akafa.
12 [e]Kenani alipokuwa ameishi miaka
sabini, akamzaa Mahalaleli. 13 Baada ya
kumzaa Mahalaleli, Kenani aliishi miaka
840, akawa na watoto wengine wa kiume
na wa kike. 14 Kenani aliishi jumla ya miaka
910, ndipo akafa.
15 Mahalaleli alipokuwa ameishi miaka
sitini na mitano, akamzaa Yaredi. 16 Baada
ya kumzaa Yaredi, Mahalaleli aliishi miaka
830, akawa na watoto wengine wa kiume
na wa kike. 17 Mahalaleli aliishi jumla ya
miaka 895, ndipo akafa.
18 [f]Yaredi alipokuwa ameishi miaka 162,
akamzaa Enoki. 19 Baada ya kumzaa Enoki,
Yaredi aliishi miaka 800, naye akawa na
watoto wengine wa kiume na wa kike.
20 Yaredi aliishi jumla ya miaka 962, ndipo
akafa.
21 [g]Enoki alipokuwa ameishi miaka sitini
na mitano, akamzaa Methusela. 22 [h]Baada
ya kumzaa Methusela, Enoki alitembea na
Mungu miaka 300, na akawa na watoto
wengine wa kiume na wa kike. 23 Enoki
aliishi jumla ya miaka 365. 24 [i]Enoki
akatembea na Mungu, kisha akatoweka,
kwa sababu Mungu alimchukua.
25 [j]Methusela alipokuwa ameishi miaka
187, akamzaa Lameki. 26 Baada ya kumzaa
Lameki, Methusela aliishi miaka 782, akawa
na watoto wengine wa kiume na wa kike.
27 Methusela aliishi jumla ya miaka 969,
ndipo akafa.
28 Lameki alipokuwa ameishi miaka 182,
alimzaa mwana. 29 [k]Akamwita jina lake Noa,
akasema, “Yeye ndiye atakayetufariji katika
kazi na maumivu makali ya mikono yetu
yaliyosababishwa na ardhi iliyolaaniwa
na BWANA.” 30 Baada ya Noa kuzaliwa,
Lameki aliishi miaka 595, akawa na watoto
wengine wa kiume na wa kike. 31 Lameki
aliishi jumla ya miaka 777, ndipo akafa.
32 [l]Baada ya Noa kuishi miaka 500,
aliwazaa Shemu, Hamu na Yafethi.

*Gharika Kuu*

6 [m]Watu walipoanza kuongezeka idadi
katika uso wa dunia na watoto wa kike
wakazaliwa kwao, 2 [n]wana wa Mungu
wakawaona kuwa hao binti za wanadamu
walikuwa wazuri wa sura, wakaoa
yeyote miongoni mwao waliyemchagua.
3 [o]Ndipo BWANA akasema, “Roho yangu
haitashindana na mwanadamu milele, kwa
kuwa yeye ni wa kufa, siku zake zitakuwa
miaka 120.”
4 [p]Wanefili walikuwako duniani siku
hizo, na baadaye, hao wana wa Mungu
walipoingia kwa binti za wanadamu na
kuzaa nao. Wanefili walikuwa mashujaa
na watu waliojulikana wa zamani hizo.

[a]**5:3** Mwa 1:26; 4:25; 1Kor 15:49; Lk 3:38
[b]**5:5** Mwa 2:17; 3:19; Ebr 9:27
[c]**5:6** Mwa 4:26; Lk 3:38
[d]**5:9** 1Nya 1:2; Lk 3:37
[e]**5:12** 1Nya 1:2; Lk 3:37
[f]**5:18** 1Nya 1:3; Lk 3:37; Yud 14
[g]**5:21** 1Nya 1:3; Lk 3:37
[h]**5:22** Mwa 6:9; 17:1; 24:40; 48:15; 2Fal 20:3; Za 116:9; Mal 2:6; Mik 6:8
[i]**5:24** 2Fal 2:1, 11; Za 49:15; 73:24; 89:48; Ebr 11:5
[j]**5:25** 1Nya 1:3; Lk 3:36
[k]**5:29** 1Nya 1:3; Lk 3:36; Mwa 3:17; Rum 8:20
[l]**5:32** Mwa 7:6, 11; 8:13; 6:10; 9:18; 10:1; Lk 3:36; 1Nya 1:4; Isa 65:20
[m]**6:1** Mwa 1:28
[n]**6:2** Ay 1:6; 2:1; Kum 21:11; Mwa 4:19
[o]**6:3** Ay 10:9; 34:14; Gal 5:15-17; Isa 40:6; 57:16; 1Pet 3:20; Za 78:39; 103:14
[p]**6:4** Hes 13:33; Mwa 11:4

5 [a]BWANA akaona jinsi uovu wa
mwanadamu ulivyokuwa mkubwa duniani,
na ya kuwa kila mwelekeo wa mawazo ya
moyo wake wakati wote ulikuwa mbaya tu.
6 [b]BWANA akasikitika kwamba alimuumba
mwanadamu duniani, moyo wa Mungu
ukajaa masikitiko. 7 [c]Kwa hiyo BWANA
akasema, “Nitamfutilia mbali mwanadamu
niliyemuumba kutoka kwenye uso wa
dunia, wanadamu na wanyama, pamoja na
viumbe vitambaavyo na ndege wa angani.
Kwa maana nasikitika kuwaumba.” 8 [d]Lakini
Noa akapata kibali machoni pa BWANA.

9 [e]Hivi ndivyo vizazi vya Noa.

Noa alikuwa mtu wa haki, na mkamilifu
miongoni mwa watu wa wakati wake, tena
alitembea na Mungu. 10 [f]Noa alikuwa na
wana watatu: Shemu, Hamu na Yafethi.

11 [g]Wakati huu dunia ilikuwa imejaa
uharibifu na ukatili machoni pa Mungu.
12 [h]Mungu akaona jinsi dunia ilivyoharibika,
kwa maana watu wote duniani walikuwa
wameharibu njia zao. 13 [i]Kwa hiyo Mungu
akamwambia Noa, “Nitawaangamiza watu
wote, kwa kuwa dunia imejaa ukatili kwa
sababu yao. Hakika mimi nitaangamiza
watu pamoja na dunia. 14 [j]Kwa hiyo
jitengenezee safina kubwa kwa mbao za
mvinje, tengeneza vyumba ndani yake na
uipake lami ndani na nje. 15 Hivi ndivyo
utakavyoitengeneza: Safina iwe na urefu
wa dhiraa 300,[k] upana wake dhiraa
hamsini[l] na kimo chake dhiraa thelathini.[m]
16 Itengenezee paa na umalizie safina kwa
kuacha nafasi ya dhiraa moja[n] juu. Weka
mlango ubavuni mwa safina, na uifanye
ya ghorofa ya chini, ya kati na ya juu.
17 [o]Nitaleta gharika ya maji juu ya nchi ili
kuangamiza uhai wote chini ya mbingu,
kila kiumbe chenye pumzi ya uhai ndani
yake. Kila kitu juu ya nchi kitaangamia.
18 [p]Lakini Mimi nitaweka Agano langu na
wewe, nawe utaingia ndani ya Safina, wewe
pamoja na mke wako, wanao na wake zao.
19 [q]Utaingiza ndani ya Safina kila aina ya
kiumbe hai wawili wawili, wa kiume na
wa kike, ili kuwahifadhi hai pamoja na
wewe. 20 [r]Wawili wa kila aina ya ndege,
wa kila aina ya mnyama na wa kila aina
ya kitambaacho ardhini watakuja kwako ili
wahifadhiwe hai. 21 Utachukua kila aina ya
chakula kitakacholiwa, na ukiweke akiba
kama chakula kwa ajili yako na yao.”

22 [s]Noa akafanya kila kitu kama vile
Mungu alivyomwamuru.

7 [t]Ndipo BWANA akamwambia Noa, “Ingia
katika safina wewe na jamaa yako yote,
kwa sababu katika kizazi hiki nimeona ya
kuwa wewe ni mwenye haki. 2 [u]Uchukue
wanyama saba walio safi wa kila aina, wa
kiume na wa kike, na wanyama wawili
wawili wa kila aina walio najisi wa kiume

[a]**6:5** Mwa 38:7; 8:21; Ay 34:26; Yer 1:16; 44:5; Eze 3:19; Za 14:1-3
[b]**6:6** Kut 32:14; 1Sam 15:11, 35; 2Sam 24:16; 1Nya 21:15; Isa 63:10; Efe 4:30; Yer 18:7-10
[c]**6:7** Eze 33:28; Sef 1:2, 18; Mwa 7:4, 21; Kut 28:36; 29:20
[d]**6:8** Eze 14:14; Mwa 19:19; 39:4; Kut 33:12-17; 34:9; Hes 11:15; Rut 2:2; Lk 1:30; Mdo 7:46
[e]**6:9** Mwa 2:4; 5:22; 7:1; 17:1; Kum 18:13; 2Sam 22:24; Ay 1:1; 4:6; 9:21; 12:4; 31:6; Za 15:2; 18:23; 19:13; 37:37; Mit 2:7; Yer 15:1; Eze 14:14-20; Dan 10:11; Lk 1:6; Ebr 11:7; 2Pet 2:5
[f]**6:10** Lk 3:36; Mwa 5:32
[g]**6:11** Kum 31:29; Amu 2:19; Za 73:6; Eze 7:23; 8:17; 28:16; Mal 2:16
[h]**6:12** Kut 32:7; Kum 4:16; 9:12, 24; Za 14:1-3
[i]**6:13** Kum 28:63; 2Fal 8:19; Ezr 9:14; Yer 44:11, 27; Mwa 7:4, 21-23; Ay 34:15; Isa 5:6; 24:1-3; Eze 7:2-3
[j]**6:14** Ebr 11:7; 1Pet 3:20; Kut 2:3

[k]15 Dhiraa 300 ni sawa na mita 135.
[l]15 Dhiraa 50 ni sawa na mita 22:5.
[m]15 Dhiraa 30 ni sawa na mita 13:5.
[n]16 Dhiraa moja ni sawa na sentimita 45.
[o]**6:17** Za 29:10; 2Pet 2:5
[p]**6:18** Mwa 7:1, 7; 9:9-16; 17:7; 19:12; Kut 6:4; 34:10; Za 25:10; 74:20; 106:45; Eze 16:60; Kum 29:13-15; Isa 55:3; Hag 2:5; Yer 32:40; 1Pet 3:20
[q]**6:19** Mwa 7:15
[r]**6:20** Mwa 7:3, 15; 1:11
[s]**6:22** Mwa 7:5; 9:16; Kut 7:6; 39:43; 40:16, 19, 21-32
[t]**7:1** Mwa 6:18; 9:6; Mt 24:38; Ebr 11:7; Lk 17:26-27; 1Pet 3:20; 2Pet 2:5; Eze 14:14
[u]**7:2** Mwa 8:20; Law 10:10; 11:1-47; Kum 14:3-20; Eze 44:23; Hag 2:12; Mdo 10:14-15

na wa kike. 3 [a]Pia uchukue ndege saba walio
safi wa kila aina, wa kiume na wa kike, ili
kuhifadhi aina zao mbalimbali katika dunia
yote. 4 [b]Siku saba kuanzia sasa nitaleta mvua
juu ya nchi kwa siku arobaini usiku na
mchana, nami nitafutilia mbali kutoka uso
wa nchi kila kiumbe hai nilichokiumba."
5 [c]Noa akafanya yote kama Bwana
alivyomwamuru.
6 [d]Noa alikuwa na miaka 600 gharika
ilipokuja juu ya dunia. 7 [e]Noa na mkewe
na wanawe na wake zao wakaingia katika
safina ili waepuke ile gharika. 8 Jozi ya
wanyama walio safi na walio najisi, ndege
na viumbe vitambaavyo, 9 [f]wa kiume na wa
kike, walikuja kwa Noa wakaingia katika
safina kama Mungu alivyomwamuru Noa.
10 Baada ya siku saba, maji ya gharika
yakaja juu ya dunia.
11 [g]Katika siku ya kumi na saba ya mwezi
wa pili mwaka wa 600 wa kuishi kwake
Noa, siku hiyo ndipo chemchemi zote hata
zilizo chini sana ya ardhi zilibubujika kwa
nguvu, na malango ya mafuriko ya mbinguni
yakafunguliwa. 12 [h]Mvua ikanyesha juu ya
nchi siku arobaini usiku na mchana.
13 [i]Siku hiyo Noa, na mkewe, na wanawe
Shemu, Hamu na Yafethi pamoja na wake
zao wakaingia katika ile safina. 14 [j]Nao
walikuwa pamoja na kila mnyama wa
mwituni kufuatana na aina yake, wanyama
wote wafugwao kufuatana na aina zao,
kila kiumbe kitambaacho juu ya ardhi
kwa aina yake, na kila ndege kufuatana
na aina yake, naam kila kiumbe chenye
mabawa. 15 [k]Viumbe vyote vyenye pumzi
ya uhai ndani yake vikaja kwa Noa viwili
viwili, vikaingia katika safina. 16 [l]Wanyama
walioingia katika safina walikuwa wa
kiume na wa kike, wa kila kiumbe chenye
uhai kama Mungu alivyomwamuru Noa,
ndipo Bwana akamfungia ndani.
17 Kwa siku arobaini mafuriko yaliendelea
kujaa duniani na maji yalivyozidi
kuongezeka, yaliinua safina juu sana kutoka
kwenye uso wa nchi. 18 Maji yakajaa na
kuongezeka sana juu ya nchi, na safina
ikaelea juu ya uso wa maji. 19 [m]Maji yakazidi
kujaa juu ya nchi, yakaifunika milima
yote mirefu chini ya mbingu yote. 20 [n]Maji
yakaendelea kujaa yakaifunika milima kwa
kina cha zaidi ya dhiraa kumi na tano.[o]
21 [p]Kila kiumbe hai kitambaacho juu ya
nchi kikaangamia: Ndege, wanyama wa
kufugwa, wanyama pori, viumbe vyote
juu ya nchi na wanadamu wote. 22 [q]Kila
kiumbe juu ya nchi kavu chenye pumzi ya
uhai kikafa. 23 [r]Kila kitu chenye uhai juu
ya uso wa nchi kilifutiliwa mbali, watu,
wanyama, viumbe vitambaavyo na ndege
warukao angani wakafutiliwa mbali toka
duniani. Waliobaki ni Noa peke yake na
wale waliokuwa pamoja naye ndani ya
safina.
24 [s]Maji yakaifunika dunia kwa siku 150.

### *Mwisho Wa Gharika*

8 [t]Mungu akamkumbuka Noa na wanyama
wote wa porini na wa kufugwa

[a]**7:3** Mwa 6:20
[b]**7:4** Mwa 2:8; 6:7, 13; 1Fal 13:34; Yer 28:16; Hes 13:25; 1Sam 17:16; 1Fal 19:8; Kut 24:18; 32:1; 34:28; Kum 9:9, 11, 18, 25; 10:10; Ay 37:6; Mt 4:2
[c]**7:5** Mwa 6:22
[d]**7:6** Mwa 5:32
[e]**7:7** Mwa 6:18
[f]**7:9** Mwa 6:22
[g]**7:11** Mwa 5:32; 8:2, 4, 14; Ay 28:11; Za 36:6; 42:7; 78:23; Mit 8:24; Isa 24:18; 51:10; Eze 26:19; 2; 2Fal 7:2; Mal 3:10
[h]**7:12** 1Sam 12:17; Ay 28:26
[i]**7:13** Mwa 8:16; 6:18; 1Pet 3:20; 2Pet 2:5
[j]**7:14** Mwa 1:11
[k]**7:15** Mwa 6:19
[l]**7:16** Mwa 6:22
[m]**7:19** Za 104:6
[n]**7:20** Mwa 8:4-5; 2Pet 3:6
[o]20 Dhiraa 15 ni sawa na mita 7.
[p]**7:21** Mwa 6:7, 13; 2Pet 3:6
[q]**7:22** Mwa 1:30
[r]**7:23** Ay 14:19; 21:18; 22:11, 16; Lk 17:27; Za 90:5; Isa 28:2; Mt 24:39; Ebr 11:7; 1Pet 3:20; 2Pet 2:5
[s]**7:24** Mwa 8:3; Ay 12:15
[t]**8:1** Mwa 9:15; 19:29; 21:1; 30:22; Kut 2:23-24; Ay 12:15; 14:13; Rut 4:13; Nah 1:4; 1Sam 1:11, 19; 2Fal 20:3; 1Nya 16:15; Neh 1:8; 5:19; 13:11-31; Hes 10:9; Za 66:6; 105:42; 106:4; Lk 1:54, 72; Kut 14:21; Yos 2:10; 3:16; Isa 11:15; 44:27

waliokuwa naye ndani ya safina, akatuma
upepo ukavuma katika dunia, nayo maji
yakaondoka. 2 [a]Zile chemchemi zilizo
chini sana ya ardhi pamoja na malango ya
mafuriko ya mbinguni yakawa yamefungwa
nayo mvua ikawa imekoma kunyesha kutoka
angani. 3 [b]Maji yakaendelea kupungua
taratibu katika nchi. Kunako mwisho wa
siku ya 150, maji yalikuwa yamepungua,
4 [c]katika siku ya kumi na saba ya mwezi wa
saba, safina ikatua katika milima ya Ararati.
5 Maji yakaendelea kupungua hadi mwezi
wa kumi, na siku ya kwanza ya mwezi wa
kumi, vilele vya milima vikaonekana.

6 Baada ya siku arobaini Noa akafungua
dirisha alilokuwa amelifanya katika safina
7 [d]na akamtoa kunguru, akawa akiruka
kwenda na kurudi mpaka maji yalipokwisha
kukauka juu ya nchi. 8 [e]Kisha akamtoa hua
ili aone kama maji yameondoka juu ya uso
wa ardhi. 9 Lakini hua hakupata mahali pa
kutua kwa kuwa maji yalienea juu ya uso
wa dunia yote, kwa hiyo akarudi kwa Noa
ndani ya safina. Noa akanyoosha mkono
akamchukua yule hua akamrudisha ndani
ya safina. 10 Noa akangojea siku saba
zaidi kisha akamtoa tena hua kutoka
safina. 11 Wakati hua aliporejea kwa Noa
jioni, alikuwa amechukua katika mdomo
wake jani bichi la mzeituni, lililochumwa
wakati ule ule! Ndipo Noa akajua ya kuwa
maji yameondoka juu ya uso wa dunia.
12 Akangojea siku saba zaidi na akamtuma
tena hua, lakini wakati huu hua hakurudi
tena kwa Noa.

13 [f]Katika siku ya kwanza ya mwezi wa
kwanza ya mwaka 601, wa kuishi kwake
Noa, maji yalikuwa yamekauka duniani.
Kisha Noa akafungua mlango wa safina
akaona ya kuwa uso wa ardhi ulikuwa
umekauka. 14 [g]Katika siku ya ishirini na saba
ya mwezi wa pili dunia ilikuwa imekauka
kabisa.

15 Ndipo Mungu akamwambia Noa,
16 [h]"Toka ndani ya safina, wewe na mkeo
na wanao na wake zao. 17 [i]Utoe nje kila aina
ya kiumbe hai aliye pamoja nawe: Ndege,
wanyama na viumbe vyote vitambaavyo
juu ya ardhi, ili wakazae, na kuongezeka
na kuijaza tena dunia."

18 [j]Kwa hiyo Noa akatoka nje pamoja na
mkewe, wanawe na wake zao. 19 Wanyama
wote na viumbe vyote vitambaavyo juu ya
ardhi na ndege wote, kila kitu kiendacho
juu ya nchi, aina moja baada ya nyingine
vikatoka katika safina, kila aina ya kiumbe,
kimoja baada ya kingine.

*Noa Atoa Dhabihu*

20 [k]Kisha Noa akamjengea BWANA
madhabahu, akachukua baadhi ya wale
wanyama na ndege wote walio safi,
akatoa sadaka za kuteketezwa juu ya
madhabahu. 21 [l]BWANA akasikia harufu
nzuri ya kupendeza, naye akasema moyoni
mwake, "Kamwe sitailaani tena ardhi kwa
sababu ya mwanadamu, hata ingawa kila
mwelekeo wa moyo wake ni mbaya tangu
ujana. Kamwe sitaangamiza tena viumbe
hai vyote kama nilivyofanya.

22 [m]"Kwa muda dunia idumupo,
wakati wa kupanda na wa kuvuna,
wakati wa baridi na wa joto,
wakati wa kiangazi na wa masika,
usiku na mchana

---

[a]**8:2** Mwa 7:4, 11
[b]**8:3** Mwa 7:24
[c]**8:4** Mwa 7:11, 20; 2Fal 19:37; Yer 51:27
[d]**8:7** Amu 11:15; Kum 14:14; 1Fal 17:4-6; Ay 38:41; Za 147:9; Mit 30:17; Isa 34:11; Lk 12:24
[e]**8:8** Ay 30:31; Za 55:6; 74:19; Wim 2:12-14; Isa 38:14; 59:11; 60:8; Yer 48:28; Eze 7:16; Nah 2:7; Hos 7:11; 11:11; Mt 3:16; 10:16; Yn 1:32
[f]**8:13** Mwa 5:32
[g]**8:14** Mwa 7:11
[h]**8:16** Mwa 7:13
[i]**8:17** Mwa 1:22
[j]**8:18** 1Pet 3:20; 2Pet 2:5
[k]**8:20** Mwa 12:7-8; 13:18; 22:9; 26:25; 33:20; 35:7; 7:8; 22:2-13; Kut 17:15; 24:4; 10:25; 20:24; 40:29; Ay 42:8; Law 1:3; 4:29; 6:8-13; Hes 6:11; Amu 6:26; 11:31; 1Sam 20:29
[l]**8:21** Kut 29:18, 25; Law 1:9, 13; 2:9; 4:31; Hes 15:3, 7; 2Kor 2:15; Mwa 3:17; 6:5; 9:11-15; Yer 17:9; Za 51:5; Mt 15:19; Rum 1:21; Yer 44:11; Isa 54:9
[m]**8:22** Yos 3:15; Za 67:6; 74:17; Yer 5:24; Zek 14:8; Mwa 1:14

kamwe havitakoma.”

*Mungu Aweka Agano Na Noa*

9 [a]Ndipo Mungu akambariki Noa
na wanawe, akiwaambia, “Zaeni
mkaongezeke kwa idadi na mkaijaze tena
dunia. 2 [b]Wanyama wote wa duniani, ndege
wote wa angani, kila kiumbe kitambaacho
juu ya ardhi, na samaki wote wa baharini
wamekabidhiwa mikononi mwenu, nao
watawaogopa na kuwahofu. 3 [c]Kila kitu
chenye uhai kiendacho kitakuwa chakula
chenu. Kama vile nilivyowapa mimea
mbalimbali, sasa nawapa kila kitu.
4 [d]“Lakini kamwe msile nyama ambayo
bado ina damu ya uhai wake, kwa maana
damu ni uhai. 5 [e]Hakika damu ya uhai wenu
nitaidai. Nitaidai kutoka kwa kila mnyama.
Kutoka kwa kila mwanadamu pia nitaidai
kwa ajili ya uhai wa mtu mwenzake.

6 [f]“Yeyote amwagaye damu ya
mwanadamu,
damu yake itamwagwa na
mwanadamu,
kwa kuwa katika mfano wa Mungu,
Mungu alimuumba mwanadamu.

7 [g]Kuhusu ninyi, zaeni mwongezeke kwa
wingi, mzidi katika dunia na kuijaza.”
8 Ndipo Mungu akamwambia Noa na
wanawe pamoja naye: 9 [h]“Sasa mimi
ninaweka Agano langu nanyi, pamoja
na uzao wenu baada yenu, 10 pia na kila
kiumbe hai kilichokuwa pamoja nanyi:
Ndege, wanyama wa kufugwa na wanyama
wote wa porini, wale wote waliotoka katika
safina pamoja nanyi, kila kiumbe hai
duniani. 11 [i]Ninaweka Agano nanyi: Kamwe
uhai hautafutwa tena kwa gharika, kamwe
haitakuwepo tena gharika ya kuangamiza
dunia.”
12 [j]Mungu akasema, “Hii ni ishara
ya Agano ninalofanya kati yangu na
ninyi na kila kiumbe hai kilicho pamoja
nanyi, Agano kwa vizazi vyote vijavyo:
13 [k]Nimeweka upinde wangu wa mvua
mawinguni, nao utakuwa ishara ya Agano
nifanyalo kati yangu na dunia. 14 Wakati
wowote ninapotanda mawingu juu ya dunia
na upinde wa mvua ukijitokeza mawinguni,
15 [l]nitakumbuka Agano langu kati yangu na
ninyi na viumbe vyote vilivyo hai vya kila
aina. Kamwe maji hayatakuwa tena gharika
ya kuangamiza uhai wote. 16 [m]Wakati wowote
upinde wa mvua unapotokea mawinguni,
nitauona na kukumbuka Agano la milele
kati ya Mungu na viumbe vyote vilivyo hai
vya kila aina duniani.”
17 Hivyo Mungu akamwambia Noa, “Hii
ndiyo ishara ya Agano ambalo nimelifanya
kati yangu na viumbe vyote vilivyo hai
duniani.”

*Wana Wa Noa*

18 [n]Wana wa Noa waliotoka ndani ya
safina ni: Shemu, Hamu na Yafethi. (Hamu
ndiye alikuwa baba wa Kanaani.) 19 [o]Hawa
ndio waliokuwa wana watatu wa Noa,
kutokana nao watu walienea katika dunia.
20 Noa akawa mkulima, akawa mtu wa
kwanza kupanda mizabibu. 21 [p]Alipokunywa
huo mvinyo wake akalewa na akalala uchi
kwenye hema lake. 22 [q]Hamu, baba wa
Kanaani, akauona uchi wa baba yake na
kuwaeleza ndugu zake wawili waliokuwa
nje. 23 Lakini Shemu na Yafethi wakachukua

[a]**9:1** Mwa 1:22
[b]**9:2** Mwa 1:26
[c]**9:3** Mwa 1:29; Kol 2:16; Mdo 10:15
[d]**9:4** Law 3:17; 7:26; 17:10-14; 19:26; Kum 12:16, 23-25; 15:23; 1Sam 14:33; Eze 33:25; Mdo 15:20, 29
[e]**9:5** Mwa 4:10; 42:22; 50:15; 1Fal 2:32; 2Nya 24:22; Za 9:12; Kut 21:28-32
[f]**9:6** Mwa 1:26; 4:14; Amu 9:24; Mt 26:52
[g]**9:7** Mwa 1:22; 9:19
[h]**9:9** Mwa 6:18
[i]**9:11** Isa 24:5; 33:8; 54:9; Hos 6:7; Mwa 8:21
[j]**9:12** Mwa 17:11-12; Kut 12:14; Law 3:17; 6:18; 17:7; Hes 10:8
[k]**9:13** Eze 1:28; Ufu 4:3; 10:1
[l]**9:15** Mwa 8:1, 21; Kut 2:24; 6:5; 34:10; Law 26:42-45; Kum 7:9; Za 89:34; 103:18; 105:8; 106:45; Eze 16:60
[m]**9:16** Mwa 17:7-13, 19; 2Sam 7:13; 23:5; Za 105:9-10; Isa 9:7; 54:10; 55:3; 59:21; 61:8; Yer 31:34; 32:40; 33:21; Eze 16:60; 37:26; Ebr 13:20
[n]**9:18** Mwa 5:32; 10:6, 15; Lk 3:36
[o]**9:19** Mwa 5:32; 1:22; 10:32; 11:4-9
[p]**9:21** Mwa 19:35
[q]**9:22** Hab 2:15

nguo wakaitanda mabegani mwao wote wawili, kisha wakaenda kinyumenyume, wakaufunika uchi wa baba yao. Nyuso zao zilielekea upande mwingine ili wasiuone uchi wa baba yao.
24 Noa alipolevuka kutoka kwenye mvinyo wake na kujua lile ambalo mwanawe mdogo kuliko wote alilokuwa amemtendea, 25 [a]akasema,

"Alaaniwe Kanaani!
Atakuwa mtumwa wa chini sana
kuliko watumwa wote kwa ndugu
zake."

26 [b]Pia akasema,

"Abarikiwe Bwana, Mungu wa
Shemu!
Kanaani na awe mtumwa wa
Shemu.
27 [c]Mungu na apanue mipaka ya
Yafethi;
Yafethi na aishi katika mahema ya
Shemu,
na Kanaani na awe mtumwa
wake."

28 Baada ya gharika Noa aliishi miaka
350. 29 [d]Noa alikuwa na jumla ya miaka
950, ndipo akafa.

*Mataifa Yaliyotokana Na Noa*

**(1 Nyakati 1:5-23)**

10 [e]Hawa ndio wazao wa Noa: Shemu, Hamu na Yafethi, ambao walizaa wana baada ya gharika.

*Wazao Wa Yafethi*

2 [f]Wana wa Yafethi walikuwa:
Gomeri, Magogu, Madai, Yavani,
Tubali, Mesheki na Tirasi.
3 [g]Wana wa Gomeri walikuwa:
Ashkenazi, Rifathi na Togarma.
4 [h]Wana wa Yavani walikuwa:
Elisha, Tarshishi, Kitimu na
Rodanimu. 5 (Kutokana na hawa
mataifa ya Pwani yalienea katika
nchi zao, kwa koo zao katika
mataifa yao, kila moja kwa lugha
yake.)

*Wazao Wa Hamu*

6 [i]Wana wa Hamu walikuwa:
Kushi, Misraimu,[j] Putu na
Kanaani.
7 [k]Wana wa Kushi walikuwa:
Seba, Havila, Sabta, Raama na
Sabteka.
Wana wa Raama walikuwa:
Sheba na Dedani.

8 [l]Kushi akamzaa Nimrodi, ambaye alikua
akawa mtu shujaa duniani. 9 [m]Alikuwa
mwindaji hodari mbele za Bwana. Ndiyo
sababu watu husema, "Kama Nimrodi,
hodari wa kuwinda mbele za Bwana."
10 [n]Vituo vyake vya kwanza katika ufalme
wake vilikuwa Babeli, Ereki, Akadi na Kalne
katika Shinari. 11 [o]Kutoka nchi ile alikwenda
Ashuru, ambako alijenga Ninawi, Rehobothiri, Kala, 12 na Reseni, iliyo kati ya Ninawi
na Kala; huo ndio mji mkubwa.

---

[a]**9:25** Mwa 27:12, 29-40; 25:23; 37:10; 49:8; Kut 20:5; Za 79:8; Isa 14:21; Yer 31:29; 32:18; Hes 24:18; Yos 9:23
[b]**9:26** Mwa 14:20; Kut 18:10; Za 7:17; 1Fal 9:21
[c]**9:27** Mwa 10:2-5; Efe 2:13-14; 3:6
[d]**9:29** Mwa 2:17
[e]**10:1** Mwa 2:4; 5:32; 1Nya 1:4
[f]**10:2** Eze 38:6; 39:1, 6; 27:13-19; 33:26; Ufu 20:8; Isa 66:19
[g]**10:3** Yer 51:27; Eze 27:13-14; 38:6
[h]**10:4** Eze 27:7, 10, 12, 25; 38:13; Za 48:7; 72:10; Isa 2:16; 23:1-6, 12; 66:19; Yer 2:10; 10:9; Yon 1:3; Hes 24:24; Dan 11:30
[i]**10:6** 2Fal 19:9; Nah 3:9; 2Nya 12:3; 16:8; Isa 11:11; 18:1; 20:3; 43:3; Yer 46:9; Eze 27:10; 30:4-9; 38:5; Mwa 9:18; Sef 2:12; 3:10
[j]6 Yaani *Misri*.
[k]**10:7** Isa 21:13; 43:3; 60:6; Mwa 2:11; 25:3; Eze 38:13; 27:15, 20, 22; 1Fal 10:1; 2Nya 9:1; Ay 1:15; 6:19; 16:11; Za 72:10; Yer 25:23-24; 6:20; 49:8; Yoe 3:8; 1Nya 1:32
[l]**10:8** Mik 5:6
[m]**10:9** 2Nya 14:9; 16:8; Isa 18:2; Mwa 25:27; 27:3
[n]**10:10** Mwa 11:2, 9; 14:1; 2Nya 36:17; Isa 10:9; 13:1; Yer 21:2; 25:12; 50:1; Ezr 4:9; Amo 6:2; Zek 5:11
[o]**10:11** Za 83:8; Isa 37:37; Mik 5:6; Sef 2:13; 2Fal 19:36; Yon 1:2; 3:2-3

[13] Misraimu alikuwa baba wa:
Waludi, Waanami, Walehabi,
Wanaftuhi, [14] [a]Wapathrusi,
Wakasluhi (hao ndio asili ya
Wafilisti), na Wakaftori.
[15] [b]Kanaani alikuwa baba wa:
Sidoni mzaliwa wake wa kwanza,
Hethi, [16] [c]Wayebusi, Waamori,
Wagirgashi, [17] [d]Wahivi, Waariki,
Wasini, [18] [e]Waarvadi, Wasemari na
Wahamathi.

Baadaye koo za Wakanaani zilitawanyika,
[19] [f]na mipaka ya Kanaani ilienea kutoka
Sidoni kuelekea Gerari hadi Gaza, kisha
kuelekea Sodoma, Gomora, Adma na
Seboimu, hadi kufikia Lasha.
[20] Hawa ni wana wa Hamu kwa koo zao
na lugha zao, katika nchi zao na mataifa
yao.

*Wazao Wa Shemu*

[21] [g]Shemu ambaye ni ndugu mkubwa wa
Yafethi, kwake kulizaliwa wana pia. Shemu
alikuwa baba wa wana wote wa Eberi.

[22] [h]Wana wa Shemu walikuwa:
Elamu, Ashuru, Arfaksadi, Ludi na
Aramu.
[23] [i]Wana wa Aramu walikuwa:
Usi, Huli, Getheri na Mesheki.
[24] [j]Arfaksadi alikuwa baba wa Shela,
naye Shela akamzaa Eberi.
[25] Eberi akapata wana wawili:
Mmoja wao aliitwa Pelegi, kwa
kuwa wakati wake ndipo dunia
iligawanyika; nduguye aliitwa
Yoktani.
[26] Yoktani alikuwa baba wa:
Almodadi, Shelefu, Hasarmawethi,
Yera, [27] [k]Hadoramu, Uzali, Dikla,
[28] [l]Obali, Abimaeli, Sheba, [29] [m]Ofiri,
Havila na Yobabu. Hawa wote
walikuwa wana wa Yoktani.

[30] Nchi waliyoishi ilienea toka Mesha
kuelekea Sefari kwenye nchi ya vilima
iliyoko mashariki.
[31] Hao ndio wana wa Shemu kwa koo zao
na lugha zao, katika nchi zao na mataifa
yao.

[32] Hizi ndizo koo za wana wa Noa,
kufuatana na vizazi vyao, katika mataifa
yao. Kutokana na hawa mataifa yalienea
duniani kote baada ya gharika.

*Mnara Wa Babeli*

11 Wakati huo dunia yote ilikuwa na
lugha moja na msemo mmoja. [2] [n]Watu
walipoelekea upande wa mashariki,
wakafika kwenye tambarare katika nchi
ya Shinari[o] nao wakaishi huko.

---

[a]**10:14** Mwa 21:32-34; 26:1, 8; Yos 13:2; Amu 3:3; Isa 14:31; Yer 47:1-4; Amo 9:7; Kum 2:23; 1Nya 1:12
[b]**10:15** Mwa 9:18; 5:20; 23:3; 25:10; 26:34; 27:46; 49:32; Yos 1:4; 11:8; Amu 10:6; Isa 23:2-4; Yer 25:22; 27:3; 47:4; Eze 16:3; 28:21; 32:30; Yoe 3:4; Zek 9:2; Kut 4:22; Hes 1:20; 3:2; 13:29; 18:15; 33:4; 1Sam 26:6
[c]**10:16** Amu 19:10; 1Nya 11:4; Ezr 9:1; Kut 3:8; 2Nya 8:7; Hes 13:29; 21:13; 32:39; Yos 2:10; Kum 1:4; 7:1; Yos 2:10; Mwa 15:18-21
[d]**10:17** Mwa 34:2; 36:2; Kut 3:8; Kum 7:1; Amu 3:3
[e]**10:18** Eze 27:8; 1Nya 18:3; Mwa 12:6; 13:17; 50:11; Kut 13:11; Hes 13:29; 14:25; 21:3; 33:40; Kum 7:1; Amu 1:1
[f]**10:19** Mwa 11:31; 12:1; 13:12; 14:2; 17:8; 24:3; 26:34; 37:1; 27:46; 28:1-8; 31:18; 35:6; 49:13; Law 25:38; Yos 19:28; Amu 1:18, 31; 18:28; 6:4; 16:1, 21; 2Nya 24:6; 14:13; Kum 2:23; 29:23; Yos 10:41; 11:22; 15:47; 1Sam 6:17; Yer 25:20; 47:1; Amo 1:6; Sef 2:4
[g]**10:21** Hes 24:24
[h]**10:22** Mwa 14:1; Isa 11:11; 21:2; Yer 25:25; 49:34; Eze 27:23; 32:24; Dan 8:2; Lk 3:36; Hes 24:22-24; Amu 3:10; 1Fal 11:25; 19:15; 20:34; 22:31; 2Fal 5:1; 8:7
[i]**10:23** Mwa 22:21; Ay 1:1; Yer 25:20; Mao 4:21
[j]**10:24** Lk 3:35
[k]**10:27** Eze 27:19
[l]**10:28** 1Fal 10:1; Ay 6:11; Za 72:10, 15; Isa 60:6; Eze 27:22
[m]**10:29** 1Fal 9:28; 1Nya 29:4; Ay 22:24; 28:16; Za 45:9; Isa 13:12; 10:32; Mwa 9:19
[n]**11:2** Mwa 10:10
[o]2 Shinari ndio Babeli.

3 [a]Wakasemezana wao kwa wao, “Njooni, tufyatue matofali na tuyachome vizuri kwa moto.” Walitumia matofali badala ya mawe, na lami kwa ajili ya kushikamanishia hayo matofali. 4 [b]Ndipo wakasema, “Njooni, tujijengee mji wenye mnara ambao utafika hadi mbinguni, ili tujipatie jina tusije tukatawanyika usoni pa dunia yote.”

5 [c]Lakini BWANA akashuka ili auone mji na mnara ambao wanadamu waliokuwa wanaujenga. 6 BWANA akasema, “Ikiwa kama taifa moja wanaozungumza lugha moja wameanza kufanya hili, basi hakuna lolote watakalopanga kufanya ambalo halitawezekana kwao. 7 [d]Njooni, tushuke tuvuruge lugha yao ili wasielewane wao kwa wao.”

8 [e]Hivyo BWANA akawatawanya kutoka mahali pale kwenda katika dunia yote, nao wakaacha kuujenga huo mji. 9 [f]Ndiyo maana pakaitwa Babeli, kwa sababu hapo ndipo BWANA alipoivuruga lugha ya dunia nzima. Kutoka hapo BWANA akawatawanya katika uso wa dunia yote.

*Shemu Hadi Abramu*

**(1 Nyakati 1:24-27)**

10 [g]Hivi ndivyo vizazi vya Shemu.

Miaka miwili baada ya gharika, Shemu alipokuwa na miaka 100, akamzaa Arfaksadi. 11 Baada ya kumzaa Arfaksadi, Shemu aliishi miaka 500, akazaa watoto wengine wa kiume na wa kike.

12 [h]Wakati Arfaksadi alipokuwa na miaka thelathini na mitano, akamzaa Shela. 13 Baada ya Arfaksadi kumzaa Shela, aliishi miaka 403, akazaa watoto wengine wa kiume na wa kike.

14 Shela alipokuwa na miaka thelathini, akamzaa Eberi. 15 Shela baada ya kumzaa Eberi, aliishi miaka 403, akazaa watoto wengine wa kiume na wa kike.

16 Eberi alipokuwa na miaka thelathini na minne, akamzaa Pelegi. 17 Baada ya Eberi kumzaa Pelegi, aliishi miaka 430, akazaa watoto wengine wa kiume na wa kike.

18 Pelegi alipokuwa na miaka thelathini, akamzaa Reu. 19 Baada ya Pelegi kumzaa Reu, aliishi miaka 209, akazaa watoto wengine wa kiume na wa kike.

20 [i]Reu alipokuwa na miaka thelathini na miwili, akamzaa Serugi. 21 Baada ya Reu kumzaa Serugi, aliishi miaka 207, akazaa watoto wengine wa kiume na wa kike.

22 [j]Serugi alipokuwa na miaka thelathini, akamzaa Nahori. 23 Baada ya Serugi kumzaa Nahori, aliishi miaka 200, akazaa watoto wengine wa kiume na wa kike.

24 [k]Nahori alipokuwa na miaka ishirini na tisa, akamzaa Tera. 25 Baada ya Nahori kumzaa Tera, aliishi miaka 119, akazaa watoto wengine wa kiume na wa kike.

26 [l]Tera alipokuwa na miaka sabini, akamzaa Abramu, Nahori na Harani.

*Wazao Wa Tera*

27 [m]Hawa ndio wazao wa Tera.

Tera aliwazaa Abramu, Nahori na Harani. Harani akamzaa Loti. 28 [n]Tera alipokuwa bado hai, Harani akafa huko Uru ya Wakaldayo, nchi alimozaliwa. 29 [o]Abramu na Nahori walioa. Mke wa Abramu aliitwa Sarai, na mke wa Nahori aliitwa Milka;

---

[a]**11:3** Kut 1:14; 5:7; Yer 43:9; Isa 9:10; Amo 5:11; Mwa 14:10
[b]**11:4** Kum 1:28; 6:10; 9:1; Ay 20:6; Yer 51:53; 31:10; 40:15; Mwa 6:4; 9:19; Kum 30:3; 4:27; 1Fal 22:17; Es 3:8; Za 44:11; Eze 6:8; Yoe 3:2
[c]**11:5** Mwa 18:21; Kut 3:6-8; 19:11, 18-20; Za 18:9; 144:5
[d]**11:7** Mwa 1:26; 42:23; Kum 28:49; Isa 28:11; 33:19; Yer 5:15; 1Kor 2:11
[e]**11:8** Mwa 9:19; Kum 32:8; Lk 1:51
[f]**11:9** Mwa 10:10; Za 55:9; Mdo 2:5-11; Isa 2:10, 21; 13:14; 24:1
[g]**11:10** Mwa 2:4; Lk 3:36
[h]**11:12** Lk 3:35
[i]**11:20** Lk 3:35
[j]**11:22** Lk 3:34
[k]**11:24** Lk 3:34
[l]**11:26** Lk 3:34; Yos 24:2; 2Fal 19:12; Isa 37:12; Eze 27:23
[m]**11:27** Mwa 2:4; 31:53; 12:4; 13:1-5, 8, 12; 14:12; 19:1; Lk 17:28; 2Pet 2:5-7
[n]**11:28** Mwa 15:7; Neh 9:7; Ay 1:17; 16:11; Eze 23:23; Mdo 7:4
[o]**11:29** Mwa 22:20-23; 24:10-24; 29:5; 12:5; 16:1; 17:15

Milka na Iska walikuwa watoto wa Harani.
30 [a]Sarai alikuwa tasa, hakuwa na watoto.
31 [b]Tera akamchukua Abramu mwanawe,
Loti mwana wa Harani mwanawe, na Sarai
mkwewe, mke wa Abramu mwanawe,
wakatoka kwa pamoja katika Uru ya
Wakaldayo kwenda nchi ya Kanaani. Lakini
walipofika Harani, wakaishi huko.
32 [c]Tera alikufa huko Harani akiwa na
miaka 205.

*Wito Wa Abramu*

12 Bwana akawa amemwambia Abramu,
"Ondoka kutoka nchi yako, uache jamii
yako na nyumba ya baba yako, uende hadi
nchi nitakayokuonyesha.

2 [d]"Mimi nitakufanya taifa kubwa
na nitakubariki,
Nitalikuza jina lako,
nawe utakuwa baraka.
3 [e]Nitawabariki wale wanaokubariki,
na yeyote akulaaniye nitamlaani;
na kupitia kwako mataifa yote
duniani
yatabarikiwa."

4 [f]Hivyo Abramu akaondoka kama
Bwana alivyokuwa amemwambia; naye
Loti akaondoka pamoja naye. Wakati
Abramu alipoitwa aondoke Harani, alikuwa
na miaka sabini na mitano. 5 [g]Abramu
akamchukua Sarai mkewe pamoja na
Loti mwana wa ndugu yake, mali zote
walizokuwa nazo pamoja na watu aliokuwa
amewapata huko Harani, wakasafiri mpaka
nchi ya Kanaani, wakafika huko.
6 [h]Abramu akasafiri katika nchi hiyo
akafika huko Shekemu, mahali penye mti
wa mwaloni ulioko More. Wakati huo
Wakanaani walikuwa wanaishi katika
nchi hiyo. 7 [i]Bwana akamtokea Abramu,
akamwambia, "Nitawapa uzao wako nchi
hii." Hivyo hapa akamjengea madhabahu
Bwana aliyekuwa amemtokea.
8 [j]Kutoka huko Abramu akasafiri kuelekea
kwenye vilima mashariki ya Betheli, naye
akapiga hema huko, Betheli ikiwa upande
wa magharibi na Ai upande wa mashariki.
Huko alimjengea Bwana madhabahu na
akaliitia jina la Bwana. 9 [k]Kisha Abramu
akasafiri kuelekea upande wa Negebu.

*Abramu Katika Nchi Ya Misri*

10 [l]Basi kulikuwako na njaa katika nchi,
naye Abramu akashuka kwenda Misri kukaa
huko kwa muda, kwa maana njaa ilikuwa
kali. 11 [m]Alipokuwa karibu kuingia Misri,

---

[a]**11:30** Mwa 16:1; 18:11; 25:21; 29:31; 30:1, 22; Amu 13:2; 1Sam 1:5; Za 113:9
[b]**11:31** Mwa 38:11; 10:19; 12:4; 27:43; 28:5-10; 29:4; Law 18:15; 20:21; Rut 1:6, 22; 2:20; 4:15; 1Sam 4:19; 1Nya 2:4; Mik 7:6; Eze 22:11; 27:23; Mdo 7:4; 2Fal 19:12
[c]**11:32** Yos 24:2
[d]**12:2** Mwa 13:16; 15:5; 17:2-4; 18:18; 22:17; 24:1, 35; 25:11; 26:3, 4; 28:3, 4, 14; 24:1, 35; 25:11; 32:12; 35:11; 41:49; 47:27; 48:16-19; 22:18; Kut 1:7; 5:5; 32:13; 20:24; Kum 1:10; 10:22; 13:17; 26:5; Yos 11:4; 24:3; 2Sam 17:11; 1Fal 3:8; 4:20; 1Nya 27:23; 2Nya 1:9; Neh 9:23; Za 107:38; 67:6; 115:12; Isa 6:13; 10:22; 48:19; 51:2; 54:3; 60:22; 19:24; Yer 4:2; 33:22; Mik 4:7; Hes 22:12; 23:8, 20; 24:9; Isa 44:3; 61:9; 65:23; Mal 3:12; Hag 2:19; Zek 8:13
[e]**12:3** Mwa 27:29; 15:5; 18:18; 22:18; 26:4; 28:4, 14; Kut 23:22; Hes 24:9; Kum 30:7; 9:5; Za 72:17; Isa 19:25; Mdo 3:25; Gal 3:8
[f]**12:4** Mwa 11:27, 31; 16:3, 16; 17:17-24; 21:5
[g]**12:5** Mwa 11:29, 31; 13:2-6; 31:18; 46:6; 14:14; 15:3; 17:23; 16:3; Mhu 2:7; Ebr 11:8
[h]**12:6** Ebr 11:9; 1Fal 12:1; Mwa 10:18; 33:18; 17:12; 35:4; Yos 17:7; 20:7; 24:26; Amu 7:1; 9:6; 8:31; 21:19; Za 60:6; 108:7
[i]**12:7** Mwa 8:20; 17:1, 8; 18:1; 26:2; 35:1; 13:4, 15-17; 15:18; 23:18; 24:7; 26:3-4; 28:13; 35:12; 48:4; 50:24; Kut 6:4-8; 6:3; 13:5, 11; 32:13; 33:1; Mdo 7:2, 5; Hes 10:29; 11:12; Kum 1:8; 2:31; 9:5; 11:9; 34:4; 30:5; Ebr 11:8; Rum 4:13; 2Fal 25:21; 1Nya 16:16; 2Nya 20:7; Za 109:9-11; Yer 25:5; Eze 47:14; Gal 3:16
[j]**12:8** Mwa 4:26; 8:20; 13:3; 28:11, 19; 26:25; 33:19; 35:1, 8, 15; Yos 7:2; 8:9; 12:9; Yer 49:3; 1Sam 7:16; 1Fal 12:29; Hos 12:4; Amo 3:14; 4:4; Ebr 11:9; Ezr 2:28; Neh 7:32
[k]**12:9** Mwa 13:1-3; 20:1; 24:62; Hes 13:17; 33:40; Kum 34:3; Yos 10:40
[l]**12:10** Mwa 41:27; 42:5; 43:1; 47:4, 13; 41:30, 54-56; 47:20; Rut 1:1; 1Sam 21:1; 2Fal 8:1; Za 105:16
[m]**12:11** Mwa 11:29; 24:16; 26:7; 29:17; 39:6

akamwambia Sarai mkewe, “Ninajua ya
kwamba wewe ni mwanamke mzuri wa
sura. 12 Wakati Wamisri watakapokuona,
watasema, ‘Huyu ni mke wake.’ Ndipo
wataniua, lakini wewe watakuacha hai.
13 [a]Sema wewe ni dada yangu, ili nitendewe
mema kwa ajili yako, na maisha yangu
yatahifadhiwa kwa sababu yako.”

14 Abramu alipoingia Misri, Wamisri
wakamwona Sarai kuwa ni mwanamke
mzuri sana wa sura. 15 Maafisa wa Farao
walipomwona, wakamsifia kwa Farao;
ndipo Sarai akapelekwa kwa nyumba
ya mfalme. 16 [b]Kwa ajili ya Sarai, Farao
akamtendea Abramu mema, naye Abramu
akapata kondoo, ng’ombe, punda, ngamia
na watumishi wa kiume na wa kike.

17 [c]Lakini Bwana akamwadhibu Farao
na nyumba yake kwa maradhi ya kufisha
kwa sababu ya kumchukua Sarai, mke wa
Abramu. 18 [d]Ndipo Farao akamwita Abramu,
akamuuliza, “Umenifanyia nini? Kwa
nini hukuniambia ni mke wako? 19 [e]Kwa
nini ulisema, ‘Yeye ni dada yangu,’ hata
nikamchukua kuwa mke wangu? Sasa basi,
mke wako huyu hapa. Mchukue uende
zako!” 20 Kisha Farao akawapa watu wake
amri kuhusu Abramu, wakamsindikiza
pamoja na mke wake na kila alichokuwa
nacho.

### *Abramu Na Loti Watengana*

13 [f]Hivyo Abramu akakwea kutoka Misri
kwenda Negebu, yeye na mkewe
na kila kitu alichokuwa nacho, pia Loti
akaenda pamoja naye. 2 [g]Wakati huo
Abramu alikuwa tajiri sana wa mifugo,
fedha na dhahabu.

3 [h]Kutoka Negebu, akapita mahali hadi
mahali, hadi akafika Betheli, mahali hapo
ambapo mwanzoni alipiga hema lake kati
ya Betheli na Ai 4 [i]hapo ambapo alikuwa
amejenga madhabahu ya kwanza. Huko
Abramu akaliitia jina la Bwana.

5 [j]Basi Loti, ambaye alikuwa anafuatana
na Abramu, alikuwa pia na makundi ya
mbuzi, kondoo, ng’ombe na mahema.
6 [k]Lakini nchi haikuwatosha kukaa pamoja
kwa ajili ya wingi wa mali zao. 7 [l]Ukazuka
ugomvi kati ya wachunga mifugo wa
Abramu na wale wa Loti. Wakati huo,
Wakanaani na Waperizi ndio waliokuwa
wenyeji wa nchi hiyo.

8 [m]Hivyo Abramu akamwambia Loti,
“Pasiwe na ugomvi wowote kati yangu na
wewe, wala kati ya wachungaji wangu na
wako, kwa kuwa sisi ni ndugu. 9 [n]Je, nchi
yote haiko mbele yako? Tutengane. Kama
ukielekea kushoto, nitakwenda kulia; kama
ukielekea kulia, mimi nitakwenda kushoto.”

10 [o]Loti akatazama akaona lile bonde
lote la Yordani kuwa lilikuwa na maji
tele, kama bustani ya Bwana, kama nchi
ya Misri, kuelekea Soari. (Hii ilikuwa kabla
Bwana hajaharibu Sodoma na Gomora.)
11 Hivyo Loti akajichagulia bonde lote la
Yordani, akaelekea upande wa mashariki.
Watu hao wawili wakatengana: 12 [p]Abramu
akaishi katika nchi ya Kanaani, wakati Loti
aliishi miongoni mwa miji ya lile bonde na
kupiga mahema yake karibu na Sodoma.
13 [q]Basi watu wa Sodoma walikuwa waovu,
wakifanya sana dhambi dhidi ya Bwana.

---

[a] **12:13** Mwa 20:2; 26:7
[b] **12:16** Mwa 24:35; 26:14; 30:43; 32:5; 34:23; 47:17; Ay 1:3; 31:25
[c] **12:17** 2Fal 15:5; Isa 53:4; Ay 30:11; 1Nya 16:21; Za 105:14
[d] **12:18** Mwa 20:9; 26:10; 29:25; 31:26; 44:15; Isa 43:27; 51:2; Eze 16:3
[e] **12:19** Mwa 20:5; 26:9
[f] **13:1** Mwa 45:25; 12:9; 11:27
[g] **13:2** Mwa 12:5; 26:13; 32:15; Mit 10:22; Ay 1:3; 42:12
[h] **13:3** Mwa 12:8-9
[i] **13:4** Mwa 12:7; 4:26
[j] **13:5** Mwa 11:27
[k] **13:6** Mwa 12:5; 33:9; 36:7
[l] **13:7** Mwa 26:20-21; 10:18; 15:20; 12:6; 34:30; Hes 20:3; Kut 3:8; Amu 1:4
[m] **13:8** Mwa 11:27; 19:9; Mit 15:18; 20:3; Kut 2:14; Hes 16:13; Za 133:1
[n] **13:9** Mwa 20:15; 34:10; 47:6; Yer 40:4
[o] **13:10** 1Fal 7:47; 2Nya 4:17; Hes 13:29; 33:48; Mwa 19:22; 2:8-10; 46:7; 14:2, 8
[p] **13:12** Mwa 10:19; 11:27; 19:17-29; 14:12
[q] **13:13** Mwa 18:20; 19:4; 19:5; 20:6; 39:9; Isa 1:10; 3:9; Hes 32:23; 1Sam 12:23; 2Sam 12:13; Za 51:4; Eze 16:49-50; 2Pet 2:8

[14] [a]Baada ya Loti kuondoka Bwana
akamwambia Abramu, “Ukiwa hapo ulipo,
inua macho yako utazame kaskazini na
kusini, mashariki na magharibi. [15] [b]Nchi yote
unayoiona nitakupa wewe na uzao wako
hata milele. [16] [c]Nitaufanya uzao wako uwe
mwingi kama mavumbi ya nchi, hivyo kama
kuna yeyote awezaye kuhesabu mavumbi,
basi uzao wako utahesabika. [17] [d]Ondoka,
tembea katika marefu na mapana ya nchi,
kwa maana ninakupa wewe.”
[18] [e]Basi Abramu akaondoa mahema yake,
akaenda kuishi karibu na mialoni ya Mamre
huko Hebroni, huko akamjengea Bwana
madhabahu.

*Abramu Amwokoa Loti*

14 [f]Wakati huu Amrafeli mfalme wa
Shinari, Arioko mfalme wa Elasari,
Kedorlaoma mfalme wa Elamu, na
Tidali mfalme wa Goimu [2] [g]kwa pamoja
walikwenda kupigana vita dhidi ya Bera
mfalme wa Sodoma, Birsha mfalme wa
Gomora, Shinabu mfalme wa Adma,
Shemeberi mfalme wa Seboimu, na
mfalme wa Bela (yaani Soari). [3] [h]Hawa
wote waliotajwa mwishoni waliunganisha
majeshi yao kutoka Bonde la Sidimu
(yaani Bahari ya Chumvi). [4] Walikuwa
wametawaliwa na Mfalme Kedorlaoma
kwa miaka kumi na miwili, lakini mwaka
wa kumi na tatu waliasi.
[5] [i]Mnamo mwaka wa kumi na nne, Mfalme
Kedorlaoma na wafalme waliojiunga naye
walikwenda kupigana na kuwashinda
Warefai katika Ashtaroth-Kanaimu,
Wazuzi katika Hamu, Waemi katika Shawe-
Kiriathaimu, [6] [j]na Wahori katika nchi ya
kilima cha Seiri, hadi El-Parani karibu
na jangwa. [7] [k]Kisha wakarudi wakaenda
En-Misfati (yaani Kadeshi), wakashinda nchi
yote ya Waamaleki, pamoja na Waamori
waliokuwa wakiishi Hasason-Tamari.
[8] [l]Ndipo mfalme wa Sodoma, mfalme
wa Gomora, mfalme wa Adma, mfalme
wa Seboimu, na mfalme wa Bela (yaani
Soari) wakatoka kupanga majeshi yao
kwenye Bonde la Sidimu [9] [m]dhidi ya
Kedorlaoma, mfalme wa Elamu, Tidali
mfalme wa Goimu, Amrafeli mfalme wa
Shinari, na Arioko mfalme wa Elasari, yaani
wafalme wanne dhidi ya wafalme watano.
[10] [n]Basi Bonde la Sidimu lilikuwa limejaa
mashimo ya lami, nao wafalme wa Sodoma
na wa Gomora walipokimbia, baadhi ya
watu walitumbukia huko na wengine
wakakimbilia vilimani. [11] Wale wafalme
wanne wakateka mali yote ya Sodoma na
Gomora pamoja na vyakula vyao vyote,
kisha wakaenda zao. [12] [o]Pia walimteka Loti
mwana wa ndugu yake Abramu pamoja
na mali zake, kwa kuwa alikuwa akiishi
Sodoma.
[13] [p]Mtu mmoja aliyekuwa ametoroka
akaja kumpa Abramu Mwebrania taarifa.
Wakati huu Abramu alikuwa anaishi
karibu na mialoni ya Mamre Mwamori,
aliyekuwa ndugu yake Eshkoli na Aneri,

---

[a]**13:14** Mwa 28:14; 32:12; 48:16; Kum 3:27; 13:17; Isa 54:3
[b]**13:15** Mwa 12:7; Gal 3:16
[c]**13:16** Mwa 12:2; 16:10; 17:20; 21:13-18; 25:16; Hes 23:10
[d]**13:17** Mwa 12:7; 15:7; Hes 13:17-25
[e]**13:18** Mwa 8:20; 14:13; 18:1; 23:2, 17, 19; 25:9; 49:30; 50:13; 35:27; Hes 13:22; Yos 10:3, 36; Amu 1:10; 1Sam 30:31; 2Sam 2:1-11; 1Nya 11:1
[f]**14:1** Mwa 10:10, 20
[g]**14:2** Mwa 10:19; 13:10
[h]**14:3** Hes 34:3-12; Kum 3:17; Yos 3:16; 12:3; 15:2-5; 18:19
[i]**14:5** Mwa 15:20; Kum 2:10, 11, 20; 3:11-13; Yos 12:4; 13:12; 17:15; 1Nya 20:4
[j]**14:6** Mwa 21:21; 36:20; 32:3; 33:14-16; 36:8; Kum 2:11, 22; Yos 11:17; 24:4; 1Nya 4:42; Isa 34:5; Eze 25:8; 35:2; Amo 1:6; Hes 12:16; 10:12; 13:3, 26; Hab 3:3
[k]**14:7** Mwa 16:14; 20:1; Hes 13:26; 20:1; 32:8; Kum 1:2; 25:17; 29:23; Yos 10:41; Amu 3:13; 6:3; 10:12; 12:15; 11:16; Za 29:8; 83:7; Kut 17:8; Hes 13:29; 14:25; 24:20; 1Sam 14:48; 15:2; 28:18; 2Sam 1:1; 1Nya 4:43; Hos 11:8
[l]**14:8** Mwa 13:10; 19:17-29; Hos 11:8; Kum 29:23
[m]**14:9** Mwa 10:22
[n]**14:10** Mwa 11:3; Za 11:1; Yos 2:16; 19:17, 30
[o]**14:12** Mwa 11:27
[p]**14:13** Mwa 13:18; 37:28; 39:14-17; 40:15; 41:12; 43:32; Kut 3:18; 1Sam 4:6; 14:11; Hes 13:23; 32:9; Kum 1:24

ambao wote walikuwa wameungana na
Abramu. 14 [a]Abramu alipopata habari
kwamba jamaa yake amechukuliwa mateka,
akawaita watu 318 wa nyumbani mwake
waliokuwa wamefunzwa kupigana vita,
wakawafuatilia hadi Dani. 15 [b]Wakati wa
usiku Abramu aliwagawa watu wake katika
vikosi ili awashambulie, na akawafuatilia,
akawafukuza hadi Hoba, kaskazini ya
Dameski. 16 [c]Akarudisha mali zote, na
akamrudisha Loti jamaa yake na mali zake,
pamoja na wanawake na watu wengine.

17 [d]Abramu aliporudi baada ya kumshinda
Mfalme Kedorlaoma na wale wafalme
waliojiunga naye, mfalme wa Sodoma
akatoka kwenda kumlaki katika Bonde la
Shawe (yaani Bonde la Mfalme).

18 [e]Ndipo Melkizedeki mfalme wa Salemu
alipoleta mkate na divai. Alikuwa kuhani wa
Mungu Aliye Juu Sana. 19 [f]Naye akambariki
Abramu, akisema,

“Abarikiwe Abramu na Mungu Aliye
Juu Sana,
Muumba wa mbingu na nchi.
20 [g]Abarikiwe Mungu Aliye Juu Sana,
ambaye amewaweka adui zako
mkononi mwako.”

Ndipo Abramu akampa Melkizedeki sehemu
ya kumi ya kila kitu.

21 Mfalme wa Sodoma akamwambia
Abramu, “Nipe hao watu na hizo mali
uchukue wewe mwenyewe.”

22 [h]Lakini Abramu akamwambia mfalme
wa Sodoma, “Nimeinua mkono wangu
kwa BWANA, Mungu Aliye Juu Sana,
Muumba wa mbingu na dunia, na nimeapa
23 [i]kwamba sitapokea kitu chochote kilicho
chako, hata kama ni uzi au gidamu ya kiatu,
ili kamwe usije ukasema, ‘Nimemtajirisha
Abramu.’ 24 [j]Sitapokea chochote, ila kile
tu watu wangu walichokula na sehemu
ambayo ni fungu la watu waliokwenda
pamoja nami, ambao ni Aneri, Eshkoli na
Mamre. Wao na wapewe fungu lao.”

### *Agano La Mungu Na Abramu*

15 [k]Baada ya jambo hili, neno la BWANA
likamjia Abramu katika maono:

“Usiogope, Abramu.
Mimi ni ngao yako,
na thawabu yako kubwa sana.”

2 [l]Lakini Abramu akasema, “Ee BWANA
Mwenyezi, utanipa nini na mimi sina hata
mtoto na atakayerithi nyumba yangu ni
huyu Eliezeri Mdameski?” 3 [m]Abramu
akasema, “Hukunipa watoto, hivyo
mtumishi katika nyumba yangu ndiye
atakuwa mrithi wangu.”

4 [n]Ndipo neno la BWANA lilipomjia:
“Mtu huyu hatakuwa mrithi wako, bali
mwana atakayetoka katika viuno vyako
mwenyewe ndiye atakayekuwa mrithi
wako.” 5 [o]Akamtoa nje na kusema, “Tazama
juu kuelekea mbinguni na uhesabu nyota,
kama hakika utaweza kuzihesabu.” Ndipo

---

[a]**14:14** Kum 4:9; 34:1; Mit 22:6; Mwa 12:5; Amu 18:29; 1Fal 15:20
[b]**14:15** Amu 1:3-8; 7:16; 15:2; 2Sam 8:5; 1Fal 20:34; 2Fal 16:9; Isa 7:8; 8:4; 10:9; 17:1; Yer 49:23, 27; Eze 27:18
[c]**14:16** 1Sam 30:8, 18
[d]**14:17** 2Sam 18:18
[e]**14:18** Za 7:8; 76:2; 104:15; 110:4; Ebr 7:2, 17, 21; 5:6; Mwa 3:19; Amu 9:13; 19:19; Es 1:10; Mit 31:6; Mhu 10:19; Wim 1:2; Dan 7:27
[f]**14:19** Ebr 7:6; Mwa 1:1; 24:3; Yos 2:11; Za 148:5; Mt 11:25
[g]**14:20** Mwa 9:26; 24:27; 28:22; Kum 14:22; 26:12; Lk 18:12; Ebr 7:4
[h]**14:22** Kut 6:8; Hes 14:30; Neh 9:15; Kum 32:40; Eze 20:5; Dan 12:7; Ufu 10:5-6
[i]**14:23** 1Sam 15:3, 19; 2Fal 5:16; Es 8:11; 9:10-15
[j]**14:24** Mwa 13:18
[k]**15:1** 1Sam 3:10; 15:10; 2Sam 7:4; 22:3, 31; 1Fal 6:11; 12:22; Yer 1:8, 13; Eze 3:16; Dan 10:1; Mwa 21:17; 26:24; 46:3; 46:2; Rut 1:20; Hes 12:6; 24:4; Ay 33:15; Kut 14:13; 20:20; 2Fal 6:16; Hag 2:5; 2Nya 20:15-17; Za 3:3; 5:12; 18:2, 20; 37:25; 58:11; 28:7; 33:20; 84:11; 119:114; 144:2; 27:1; Isa 7:4; 41:10-14; 43:1, 5; Kum 33:29; Mit 2:7; 30:5
[l]**15:2** Isa 49:22; Yer 44:26; Eze 5:11; 16:48; Mdo 7:5; Mwa 14:15
[m]**15:3** Mwa 24:2, 34; 12:5
[n]**15:4** Gal 4:28
[o]**15:5** Ay 11:8; 35:5; Za 8:3; 147:4; Yer 30:19; 33:22; Mwa 12:2; Rum 4:18; Ebr 11:12; Kut 32:13

akamwambia, “Hivyo ndivyo uzao wako
utakavyokuwa.”
6 [a]Abramu akamwamini BWANA, naye
kwake hili likahesabiwa kuwa haki.
7 [b]Pia akamwambia, “Mimi ndimi BWANA,
niliyekutoa toka Uru ya Wakaldayo nikupe
nchi hii uimiliki.”
8 [c]Lakini Abramu akasema, “Ee BWANA
Mwenyezi, nitawezaje kujua kwamba
nitapata kuimiliki?”
9 [d]Ndipo BWANA akamwambia, “Niletee
mtamba wa ng’ombe, mbuzi na kondoo
dume, kila mmoja wa miaka mitatu, pamoja
na hua na kinda la njiwa.”
10 [e]Abramu akamletea hivi vyote,
akampasua kila mnyama vipande viwili,
akavipanga kila kimoja kuelekea mwenzake,
lakini hata hivyo ndege, hakuwapasua
vipande viwili. 11 [f]Kisha ndege walao nyama
wakatua juu ya mizoga, lakini Abramu
akawafukuza.
12 [g]Wakati jua lilipokuwa linatua, Abramu
akashikwa na usingizi mzito, giza nene na
la kutisha likaja juu yake. 13 [h]Kisha BWANA
akamwambia, “Ujue hakika kwamba wazao
wako watakuwa wageni kwenye nchi
ambayo si yao, nao watafanywa watumwa
na kuteswa kwa miaka mia nne. 14 [i]Lakini
nitaliadhibu taifa lile watakalolitumikia
kama watumwa, na baadaye watatoka
huko na mali nyingi. 15 [j]Wewe, hata hivyo
utakwenda kwa baba zako kwa amani na
kuzikwa katika uzee mwema. 16 [k]Katika
kizazi cha nne wazao wako watarudi hapa,
kwa maana dhambi ya Waamori bado
haijafikia kipimo kilichojaa.”
17 [l]Wakati jua lilipokuwa limezama na
giza limeingia, tanuru la moshi na mwali
wa moto unaowaka vikatokea na kupita
kati ya vile vipande vya nyama. 18 [m]Siku
hiyo BWANA akafanya Agano na Abramu,
na kumwambia, “Nitawapa wazao wako
nchi hii, kuanzia Kijito cha Misri[n] hadi
mto ule mkubwa, Frati, 19 [o]yaani nchi ya
Wakeni, Wakenizi, Wakadmoni, 20 [p]Wahiti,
Waperizi, Warefai, 21 [q]Waamori, Wakanaani,
Wagirgashi na Wayebusi.”

### *Hagari Na Ishmaeli*

16 [r]Basi Sarai, mkewe Abramu, alikuwa
hajamzalia watoto. Lakini alikuwa na
mtumishi wa kike Mmisri jina lake Hagari,
2 [s]hivyo Sarai akamwambia Abramu,
“BWANA amenizuilia kupata watoto.
Nenda, ukakutane kimwili na mtumishi
wangu wa kike, huenda nitaweza kupata
watoto kupitia kwake.”
Abramu akakubaliana na lile Sarai
alilosema. 3 [t]Hivyo baada ya Abramu kuishi
katika nchi ya Kanaani miaka kumi, Sarai
akamchukua mtumishi wake wa kike wa
Kimisri, Hagari na kumpa mumewe awe

---

[a]**15:6** Za 106:31; Rum 4:3, 20-24; Gal 3:6; Yak 2:23
[b]**15:7** Mwa 12:1; 13:17; 17:8; 28:4; 35:12; 48:4; Kut 6:8; 20:2; Mdo 7:3; Ebr 11:8; Kum 9:5
[c]**15:8** Lk 1:18; Kum 12:20; 19:8
[d]**15:9** Hes 19:2; Kum 21:3; Hos 4:16; Amo 4:1; 1Sam 1:24; Law 1:14; 5:7, 11; 12:8
[e]**15:10** Yer 34:18; Law 1:17; 5:8
[f]**15:11** Kum 28:26; Yer 7:33
[g]**15:12** Mwa 2:21
[h]**15:13** Kut 1:11; 3:7; 5:6-14; 12:40; Ay 3:18; Kum 5:15; Mdo 7:6; Hes 20:15; Gal 3:17
[i]**15:14** Mwa 50:24; Kut 3:8; 6:6-8; 12:25; 12:32-38; Hes 10:29; Yos 1:2; Mdo 7:7
[j]**15:15** Mwa 25:8; 35:29; 47:30; 49:29; Kum 31:16; 34:7; 2Sam 7:12; 1Fal 1:21; Za 49:19; 91:16; Kut 23:29; Yos 14:11; Amu 8:32; 1Nya 29:28; Ay 5:26; 21:23; 42:17; Mit 3:16; 9:11; Isa 65:20
[k]**15:16** Kut 3:8, 17; 12:40; Mwa 28:15; 46:4; 48:21; 50:24; Law 18:28; Yos 13:4; Amu 10:11; Eze 16:3; 1Fal 21:26; 2Fal 16:3; 21:11
[l]**15:17** Amu 7:16-20; 14:4-5
[m]**15:18** Mwa 2:14; 4:7; 12:7; 17:2-7; Kut 6:4; 34:10, 27; 1Nya 16:16; Za 105:9; Hes 34:5; Isa 27:12; Yos 15:4, 47; 1Fal 8:65; 2Fal 24:7; 2Nya 7:8; Yer 37:5; 46:2; Mao 4:17; Eze 30:22; 47:19
[n]18 *Kijito cha Misri* hapa ina maana *Wadi-el-Arish* kwenye mpaka wa kusini wa Yuda.
[o]**15:19** Hes 24:21; Amu 1:16; 4:11; 5:24; 1Sam 15:6; 27:10; 30:29; 1Nya 2:55
[p]**15:20** Mwa 10:15; Kum 7:1; Mwa 13:7; 14:5
[q]**15:21** Mwa 10:16; Yos 3:10; 24:11; Neh 9:8
[r]**16:1** Mwa 11:29, 30; 24:61; 29:24-29; 31:33; 46:18; 21:14; 25:12; 30:2; Lk 1:7, 36; Gal 4:24-25
[s]**16:2** Mwa 19:31-32; 30:3-10
[t]**16:3** Mwa 12:4-5

mke wake. 4 [a]Akakutana kimwili na Hagari,
naye akapata mimba.
Hagari alipojua kuwa ana mimba,
alianza kumdharau Sarai. 5 [b]Ndipo Sarai
akamwambia Abramu, “Unawajibika na
manyanyaso ninayoyapata. Nilimweka
mtumishi wangu mikononi mwako, sasa
kwa vile anajua kwamba ana mimba,
ananidharau mimi. BWANA na aamue kati
yako na mimi.”
6 [c]Abramu akamwambia, “Mtumishi wako
yuko mikononi mwako. Mtendee lolote
unalofikiri ni bora zaidi.” Ndipo Sarai
akamtesa Hagari, hivyo akamtoroka.
7 [d]Malaika wa BWANA akamkuta Hagari
karibu na chemchemi huko jangwani;
ilikuwa chemchemi ile iliyokuwa kando
ya barabara iendayo Shuri. 8 [e]Malaika
akamwambia, “Hagari, mtumishi wa Sarai,
umetokea wapi, na unakwenda wapi?”
Akamjibu, “Ninamkimbia bibi yangu
Sarai.”
9 Ndipo malaika wa BWANA akamwambia,
“Rudi kwa bibi yako ukajishushe chini
yake.” 10 [f]Malaika akaendelea akasema,
“Nitazidisha wazao wako, hivi kwamba
watakuwa wengi mno wasiohesabika.”
11 [g]Pia malaika wa BWANA akamwambia:

“Wewe sasa una mimba
nawe utamzaa mwana.
Utamwita jina lake Ishmaeli,[h]
kwa sababu BWANA amesikia juu
ya huzuni yako.
12 [i]Atakuwa punda-mwitu katikati ya
wanadamu,
mkono wake utakuwa dhidi ya
kila mtu
na mkono wa kila mtu dhidi yake,
naye ataishi kwa uhasama
na ndugu zake wote.”

13 [j]Hagari akampa BWANA aliyezungumza
naye jina hili: “Wewe ndiwe Mungu
unionaye mimi,” kwa maana alisema,
“Sasa nimemwona yeye anayeniona mimi.”
14 [k]Ndiyo sababu kisima kile kikaitwa Beer-
Lahai-Roi,[l] ambacho bado kipo huko hata
leo kati ya Kadeshi na Beredi.
15 [m]Hivyo Hagari akamzalia Abramu
mwana, naye Abramu akamwita huyo
mwana Hagari aliyemzalia, Ishmaeli.
16 [n]Abramu alikuwa na umri wa miaka
themanini na sita wakati Hagari alipomzalia
Ishmaeli.

*Agano La Tohara*

17 [o]Abramu alipokuwa na miaka tisini na
tisa, BWANA akamtokea akamwambia,
“Mimi ndimi Mungu Mwenyezi;[p] enenda
mbele zangu na uishi kwa unyofu. 2 [q]Nami
nitafanya Agano langu kati yangu na wewe,
nami nitakuzidisha sana sana.”

---

[a]**16:4** Mwa 30:1; 1Sam 1:6
[b]**16:5** Mwa 31:53; Kut 5:21; Amu 11:27; 1Sam 24:12-15; 26:10, 23; Za 50:6; 75:7
[c]**16:6** Yos 9:25; Mwa 31:50
[d]**16:7** Mwa 21:17; 22:11-15; 24:7, 40; 25:18; 31:11; 48:16; Kut 3:2; 14:19; 15:22; 23:20-23; 32:34; 33:2; Amu 2:1; 6:11; 13:3; Za 34:7; 2Sam 24:16; 21:19; 1Fal 19:5; 2Fal 1:3; 19:35; Zek 1:11; Mdo 5:19; 1Sam 15:7
[e]**16:8** Mwa 3:9
[f]**16:10** Mwa 13:16; 17:20
[g]**16:11** Mdo 5:19; Mwa 3:15; 12:2-3; 18:19; 17:19; 21:3; 37:25-28; 29:32; 31:42; Neh 9:7; Isa 44:1; Amo 3:2; Mt 1:21; Lk 1:13, 31; Amu 8:24; Kut 2:24; 3:7, 9; 4:31; Hes 20:16; Kum 26:7; 1Sam 9:16
[h]11 Ishmaeli maana yake Mungu husikia.
[i]**16:12** Ay 6:5; 11:12; 24:5; 39:5; Hos 8:9; Za 104:11; Yer 2:24; Mwa 25:18
[j]**16:13** Za 139:1-12; Mwa 32:30; 33:10; Kut 24:10; 33:20-23; Hes 12:8; Amu 6:22; 13:22; Isa 6:5
[k]**16:14** Mwa 24:62; 25:11; 14:7
[l]14 Beer-Lahai-Roi maana yake Yeye Aliye Hai Anionaye Mimi.
[m]**16:15** Mwa 21:9; 17:18; 25:12; 28:9; Gal 4:22
[n]**16:16** Mwa 12:4
[o]**17:1** Mwa 5:22; 12:4-7; 20:5; 28:3; 35:11; 43:14; 48:3; 49:25; Kut 6:3; 18:13; Rut 1:20; Ay 5:17; 6:4, 14; 22:21; 33:19; 36:16; Isa 13:6; Yoe 1:15; Mik 6:9; 1Fal 3:6; 9:4; Za 15:2; 18:23; 78:72; 101:2
[p]1 Mungu Mwenyezi hapa ni jina la Kiebrania, El-Shaddai (yaani Mungu Mwenye utoshelevu wote).
[q]**17:2** Mwa 12:2; 15:18; 22:16-18

3 [a]Abramu akaanguka kifudifudi, naye
Mungu akamwambia, 4 [b]"Kwa upande
wangu, hili ndilo Agano langu na wewe:
Wewe utakuwa baba wa mataifa mengi.
5 [c]Jina lako hutaitwa tena Abramu, bali
jina lako litakuwa Abrahamu,[d] kwa maana
nimekufanya wewe baba wa mataifa mengi.
6 [e]Nitakufanya uwe na uzao mwingi sana,
kwako yatatoka mataifa nao wafalme
watatoka kwako. 7 [f]Nitalithibitisha Agano
langu kama Agano la milele kati yangu
na wewe na wazao wako baada yako na
vizazi vijavyo niwe Mungu wako na Mungu
wa wazao wako. 8 [g]Nchi yote ya Kanaani,
unakoishi sasa kama mgeni, nitakupa kuwa
milki yako milele, na uzao wako, nami
nitakuwa Mungu wao."

9 [h]Ndipo Mungu akamwambia Abrahamu,
"Kwa upande wako, lazima ushike
Agano langu, wewe na wazao wako kwa
ajili ya vizazi vijavyo. 10 [i]Hili ni Agano
langu na wewe pamoja na wazao wako
baada yako, Agano mtakalolishika: Kila
mwanaume miongoni mwenu atatahiriwa.
11 [j]Mtafanyiwa tohara na hii itakuwa
ni alama ya Agano kati yangu na ninyi.
12 [k]Kwa vizazi vijavyo, kila mwanaume
miongoni mwenu mwenye siku nane ni
lazima atahiriwe, pamoja na watakaozaliwa
nyumbani mwako au walionunuliwa kwa
fedha kutoka kwa mgeni, wale ambao sio
watoto wako. 13 [l]Awe amezaliwa nyumbani
mwako au amenunuliwa kwa fedha yako,
ni lazima watahiriwe. Agano langu katika
mwili wako litakuwa ni Agano la milele.
14 [m]Kila mwanaume asiyetahiriwa, ambaye
hajapata tohara ya mwilini, atatengwa na
watu wake, amelivunja Agano langu."

15 [n]Pia BWANA akamwambia Abrahamu,
"Kwa upande wa Sarai mkeo, hutamwita
tena Sarai bali jina lake litakuwa Sara.
16 [o]Nitambariki na hakika nitakupatia
mwana kwake. Nitambariki na kwamba
atakuwa mama wa mataifa, wafalme wa
mataifa watatoka kwake."

17 [p]Abrahamu akaanguka kifudifudi,
akacheka na kusema moyoni mwake, "Je,
mtu wa miaka mia moja aweza kuzaa
mwana? Je, Sara atazaa mtoto katika
umri wa miaka tisini?" 18 [q]Abrahamu
akamwambia Mungu, "Laiti Ishmaeli naye
angeshiriki baraka yako!"

19 [r]Ndipo Mungu akasema, "Ndiyo, lakini
mkeo Sara atakuzalia wewe mwana, nawe
utamwita jina lake Isaki.[s] Nitalithibitisha
Agano langu naye kama Agano la milele
kwa ajili yake na wazao wake baada yake.
20 [t]Kwa upande wa Ishmaeli, nimekusikia:
hakika nitambariki, nitamfanya awe na

---

[a]**17:3** Mwa 18:2; 19:1; 33:3; Kut 18:7; Hes 14:5; Yos 5:14; 7:6; Amu 13:20; Eze 1:28; 3:23
[b]**17:4** Mwa 15:18; 12:2; 25:23
[c]**17:5** Mwa 32:28; 35:10; 37:3, 13; 43:6; 46:2; 1Fal 18:31; 2Fal 17:34; 1Nya 1:34; Neh 9:7; Isa 48:1; Yn 1:42; Rum 4:17
[d]5 Abrahamu maana yake Baba wa watu wengi.
[e]**17:6** Mwa 1:28; 18:10; 21:1; 22:17; 26:22; 28:3; 35:11; 36:31; 41:52; 47:27; 48:4; 49:22; Law 26:9; Mt 1:6; Kum 7:13; Isa 51:2
[f]**17:7** Mwa 6:18; 9:16; 18:15; Kut 6:7; 20:2; 29:45-46; Law 11:44-45; 18:2; 22:33; 25:38; 26:9, 12, 15; Hes 15:41; Kum 4:20; 7:6, 21; 29:13; 2Sam 7:24; Ebr 13:20; Yer 14:9; Ufu 21:7; Rum 9:8; Gal 3:16
[g]**17:8** Mwa 10:19; 12:7; 15:7; 23:4; 28:4; 35:27; 37:1; Kut 6:4; Yer 31:1; 1Nya 29:15
[h]**17:9** Mwa 18:19; 22:18; Kut 19:5; Kum 5:2
[i]**17:10** Mwa 21:4; Law 12:3; Yos 5:2-7; Rum 4:11; Yn 7:22; Mdo 7:8
[j]**17:11** Kut 12:48; Kum 10:16; Mwa 9:12; Rum 4:11
[k]**17:12** Mwa 9:12; 21:4; Law 12:3; Yos 5:2; Lk 1:59; 2:21
[l]**17:13** Kut 12:44-48; Mwa 9:16
[m]**17:14** Kut 4:24-26; 12:15, 19; 30:33; Eze 44:7; Yos 5:2-8; Law 7:20, 25; 17:4; 18:29; 19:8; 20:17; Hes 9:13; 15:30; 19:13; Kum 17:12; Ay 38:15; Za 37:28
[n]**17:15** Mwa 11:29
[o]**17:16** Mwa 18:10; 24:60; Isa 29:22; Gal 4:31
[p]**17:17** Mwa 12:4; 18:11-13; 21:6, 7; 24:1, 36; Yer 20:15; Lk 1:18; Rum 4:19; Gal 4:23; Ebr 11:11
[q]**17:18** Mwa 16:15; 21:11
[r]**17:19** Mwa 9:16; 16:11; 18:14; 21:2; 26:3; 50:24; Kut 13:11; Kum 1:8; Gal 3:16; 1Sam 1:20; Mt 1:21; Lk 1:13, 31
[s]19 Isaki maana yake Kucheka.
[t]**17:20** Mwa 13:16; 16:10; 25:12-18; 48:19

uzao mwingi na nitaongeza sana idadi
yake. Atakuwa baba wa watawala kumi na
wawili, nami nitamfanya awe taifa kubwa.
21 [a]Lakini Agano langu nitalithibitisha kwa
Isaki, ambaye Sara atakuzalia mwaka ujao
majira kama haya." 22 [b]Wakati alipomaliza
kuzungumza na Abrahamu, Mungu
akapanda juu akaondoka kwa Abrahamu.
23 [c]Siku ile ile, Abrahamu akamchukua
Ishmaeli mwanawe na wote waliozaliwa
nyumbani mwake pamoja na walionunuliwa
kwa fedha zake, kila mwanaume wa
nyumbani mwake, akawatahiri, kama
Mungu alivyomwagiza. 24 [d]Abrahamu
alikuwa na umri wa miaka tisini na tisa
alipotahiriwa, 25 [e]naye Ishmaeli mwanawe
alitahiriwa akiwa na umri wa miaka
kumi na mitatu. 26 Abrahamu na Ishmaeli
mwanawe walitahiriwa siku ile ile, 27 [f]Kila
mwanaume nyumbani mwa Abrahamu,
pamoja na wote waliozaliwa nyumbani
mwake au aliyenunuliwa kwa fedha kutoka
kwa mgeni, alitahiriwa pamoja naye.

*Wageni Watatu*

18 [g]BWANA akamtokea Abrahamu karibu
na mialoni ya Mamre wakati alipokuwa
ameketi kwenye ingilio la hema lake wakati
wa adhuhuri. 2 [h]Abrahamu akainua macho
akaona watu watatu wamesimama karibu
naye. Alipowaona, aliharakisha kutoka
kwenye ingilio la hema lake kuwalaki na
kuwasujudia hadi nchi.
3 Akasema, "Kama nimepata kibali
machoni penu, ee bwana wangu, usimpite
mtumishi wako. 4 [i]Acha yaletwe maji
kidogo, kisha ninyi nyote mnawe miguu
yenu na mpumzike chini ya mti huu.
5 [j]Niruhusuni niwapatie chakula kidogo
mle, ili mpate nguvu mwendelee na safari
yenu, kwa kuwa mmekuja kwa mtumishi
wenu."

Nao wakamjibu, "Vema sana, fanya kama
unavyosema."

6 [k]Hivyo Abrahamu akaharakisha akaingia
hemani kwa Sara, akamwambia, "Chukua
vipimo vitatu vya unga laini haraka, ukande
na uoke mikate."
7 [l]Kisha Abrahamu akakimbia kwenda
kwenye kundi, akachagua ndama mzuri,
laini na akampa mtumishi, ambaye
aliharakisha kumtayarisha. 8 [m]Kisha akaleta
jibini, maziwa na nyama ya yule ndama
iliyoandaliwa, akaviweka mbele ya wageni.
Walipokuwa wakila, alisimama karibu nao
chini ya mti.
9 [n]Wakamuuliza, "Yuko wapi Sara mkeo?"

Akasema, "Yuko huko, ndani ya hema."

10 [o]Kisha BWANA akasema, "Hakika
nitakurudia tena majira kama haya mwakani
na Sara mkeo atakuwa ana mwana."

Sara alikuwa akiwasikiliza kwenye
ingilio la hema, lililokuwa nyuma yake.
11 [p]Abrahamu na Sara walikuwa wazee
tena waliosogea miaka, naye Sara alikuwa
amekoma katika desturi ya wanawake.
12 [q]Hivyo Sara akacheka kimoyomoyo
alipokuwa akiwaza, "Baada ya mimi kuwa
mkongwe hivi na bwana wangu amezeeka,
je, nitaweza kufurahia jambo hili?"
13 [r]Ndipo BWANA akamwambia
Abrahamu, "Kwa nini Sara amecheka na
kusema, 'Kweli nitazaa mtoto nami sasa
ni mzee?' 14 [s]Je, kuna jambo lolote gumu
lisilowezekana kwa BWANA? Nitakurudia

---

[a]**17:21** Kut 34:10; Mwa 18:10-14; 21:2
[b]**17:22** Mwa 18:33; 35:13; Hes 12:9
[c]**17:23** Mwa 12:5
[d]**17:24** Mwa 12:4; Rum 4:11
[e]**17:25** Mwa 16:16
[f]**17:27** Mwa 14:14
[g]**18:1** Mwa 12:7; 13:18; 14:13; 19:1; 23:10, 18; 34:20-24; Rut 4:1; Ebr 11:9; Za 69:12
[h]**18:2** Mwa 17:2-3; 19:1, 10; 24:63; 32:24; 43:28; Yos 5:13; Ebr 13:2; Amu 13:6-11; Hos 12:2-4
[i]**18:4** Mwa 19:2; 24:32; 43:24; Amu 19:21; 2Sam 11:8; Lk 7:44
[j]**18:5** Amu 13:15; 19:5
[k]**18:6** Mwa 19:3; 2Sam 13:8
[l]**18:7** 1Sam 28:24; Lk 15:23
[m]**18:8** Isa 7:15, 22; Amu 4:19; 5:25; 6:19
[n]**18:9** Mwa 3:9; 24:67; Ebr 11:9
[o]**18:10** Mwa 17:6, 21; 21:2; 2Fal 4:16; Rum 6:6
[p]**18:11** Mwa 11:30; 17:17; Lk 1:18; Rum 4:19; Ebr 11:11-12
[q]**18:12** Mwa 17:17; 21:6; 1Pet 3:6
[r]**18:13** Mwa 17:17
[s]**18:14** Ay 42:2; Isa 40:29; 50:2; 51:9; Gal 4:23; Yer 32:17; Mt 19:26; Rum 4:21; 9:9; Mwa 17:19

mwakani majira kama haya, naye Sara atakuwa na mwana."

15 Sara akaogopa kwa kuwa alidanganya na kusema, "Mimi sikucheka."

Lakini Bwana akasema, "Ndiyo, ulicheka!"

*Abrahamu Aiombea Sodoma*

16 Wakati watu hao waliposimama ili waondoke, walielekeza nyuso zao Sodoma, Abrahamu akawatoa kitambo kidogo ili awasindikize. 17 [a]Ndipo BWANA akasema, "Je, nimfiche Abrahamu jambo ninalokusudia kufanya? 18 [b]Hakika Abrahamu atakuwa taifa kubwa na lenye nguvu, kupitia kwake mataifa yote ya dunia yatabarikiwa. 19 [c]Kwa maana nimemchagua yeye, ili awaongoze watoto wake na jamaa yake kufuata njia ya BWANA, kwa kuwa waadilifu na kutenda haki, ili BWANA atimize ahadi yake kwa Abrahamu."

20 [d]Basi BWANA akasema, "Kilio dhidi ya Sodoma na Gomora ni kikubwa sana na dhambi yao inasikitisha sana, 21 [e]kwamba nitashuka nione kama waliyoyatenda ni mabaya kiasi cha kilio kilichonifikia. Kama sivyo, nitajua."

22 [f]Basi wale watu wakageuka wakaenda kuelekea Sodoma, lakini Abrahamu akabaki amesimama mbele za BWANA. 23 [g]Ndipo Abrahamu akamsogelea akasema: "Je, utawaangamiza wenye haki na waovu? 24 [h]Je, ikiwa watakuwepo watu wenye haki hamsini katika mji huo, hivi kweli utauangamiza na wala hutauacha kwa ajili ya hao watu hamsini wenye haki waliomo ndani yake? 25 [i]Hilo na liwe mbali nawe, kufanya jambo kama hilo, kuwaua wenye haki pamoja na waovu, kuwatendea wenye haki sawasawa na waovu. Iwe mbali nawe! Je, Mwamuzi wa dunia yote hatafanya lililo sawa?"

26 BWANA akasema, "Kama nikipata watu hamsini wenye haki katika mji wa Sodoma, nitausamehe huo mji wote kwa ajili yao."

27 [j]Kisha Abrahamu akasema tena: "Sasa kwa kuwa nimekuwa na ujasiri wa kuzungumza na Bwana, ingawa mimi si kitu bali ni mavumbi na majivu; 28 je, kama hesabu ya wenye haki imepungua watano katika hamsini, utauangamiza huo mji wote kwa ajili ya hao watano waliopungua?"

Bwana akamwambia, "Kama nikiwakuta huko watu arobaini na watano, sitauangamiza."

29 Abrahamu akazungumza naye kwa mara nyingine, "Je, kama huko watapatikana watu arobaini tu?"

Akamjibu, "Kwa ajili ya hao arobaini, sitauangamiza."

30 [k]Ndipo akasema, "Bwana na asikasirike, lakini niruhusu nizungumze. Je, kama huko watakuwepo thelathini tu?"

Akajibu, "Sitapaangamiza ikiwa nitawakuta huko watu thelathini."

31 Abrahamu akasema, "Sasa kwa kuwa nimekuwa na ujasiri sana kuzungumza na Bwana, je, kama wakipatikana huko watu ishirini tu?"

Bwana akajibu, "Kwa ajili ya hao ishirini, sitauangamiza."

32 [l]Abrahamu akasema, "Bwana na asikasirike, lakini niruhusu nizungumze tena mara moja tu. Itakuwaje kama watapatikana huko watu kumi tu?"

Bwana akajibu, "Kwa ajili ya hao kumi, sitauangamiza."

[a]**18:17** Amo 3:7; Mwa 19:24; Ay 1:16; Za 107:34
[b]**18:18** Mwa 12:2; Gal 3:8
[c]**18:19** Mwa 16:11; 17:9; 22:12, 18; 26:5; Kum 4:9-10; 6:7; Isa 14:1; Efe 6:4; Yos 24:15; Yer 23:5; 2Sam 8:15; Za 17:2; 99:4
[d]**18:20** Isa 1:10; Yer 23:14; Eze 16:46; Mwa 13:13; 19:13
[e]**18:21** Mwa 11:5
[f]**18:22** Mwa 19:1, 27
[g]**18:23** Kut 23:7; 2Pet 2:9; Law 4:3, 22, 27; Hes 16:22; Eze 18:4; Kum 27:25; 2Sam 24:17; Za 11:4-7; 94:21
[h]**18:24** Yer 5:1
[i]**18:25** Mwa 20:4; 44:7; Kum 32:4; 1:16-17; Rum 3:6; Ay 8:3-7; 9:15; 34:10; 36:23; Isa 3:10-11; 5:20; Amo 5:15; Mal 2:17; 3:18; Amu 11:27; Za 7:11; 58:11; 75:7; 94:2; 119:137; Ebr 12:23; 2Nya 19:7; Ezr 9:15; Neh 9:33; Eze 18:25; Dan 4:37; 9:14
[j]**18:27** Mwa 2:7; Ay 2:8
[k]**18:30** Mwa 44:18; Kut 32:22
[l]**18:32** Amu 6:39; Yer 5:1

33 [a]BWANA alipomaliza kuzungumza na
Abrahamu, akaondoka, naye Abrahamu
akarudi nyumbani kwake.

### *Kuangamizwa Kwa Sodoma Na Gomora*

19 [b]Malaika wale wawili wakafika Sodoma
wakati wa jioni, naye Loti alikuwa
ameketi kwenye lango la mji. Wakati
alipowaona, aliondoka kwenda kuwalaki
na kuwasujudia hadi chini. 2 [c]Akasema,
"Bwana zangu, tafadhali karibuni kwenye
nyumba ya mtumishi wenu. Mnaweza
kunawa miguu na kulala hapa kisha asubuhi
na mapema mwendelee na safari yenu."
Wakamjibu, "La hasha, tutalala hapa nje
uwanjani."
3 [d]Lakini akasisitiza kwa nguvu kwamba
waingie pamoja naye nyumbani kwake.
Akawaandalia chakula, mikate isiyotiwa
chachu, nao wakala. 4 [e]Kabla hawajaenda
kulala, watu wote kutoka kila sehemu
ya mji wa Sodoma, vijana kwa wazee,
waliizunguka nyumba. 5 [f]Wakamwita Loti
wakisema, "Wako wapi wale watu ambao
walikuja kwako jioni hii? Watoe nje kwetu
ili tuweze kuwalawiti."
6 [g]Loti akatoka nje kuonana nao,
akaufunga mlango nyuma yake, 7 akasema,
"La hasha, rafiki zangu. Msifanye jambo
hili ovu. 8 [h]Tazama, ninao binti wawili
ambao kamwe hawajakutana kimwili na
mwanaume. Acha niwatoe nje kwenu, nanyi
mnaweza kuwafanyia lolote mnalotaka.
Lakini msiwafanyie chochote watu hawa,
kwa sababu wako kwenye ulinzi chini ya
dari langu."
9 [i]Wakamjibu, "Tuondokee mbali."
Wakaendelea kusema, "Huyu mtu alikuja
hapa kama mgeni na sasa anataka kuwa
mwamuzi wetu! Tutakutenda vibaya kuliko
wao." Waliendelea kumlazimisha Loti na
kusonga mbele ili kuvunja mlango.
10 [j]Lakini watu wale waliokuwa ndani
wakanyoosha mkono wakamvuta Loti
ndani ya nyumba na kufunga mlango.
11 [k]Kisha wakawapiga kwa upofu wale watu
waliokuwa mlangoni mwa ile nyumba,
vijana kwa wazee, hivyo hawakuweza
kuupata mlango.
12 [l]Wale watu wawili wakamwambia Loti,
"Una mtu mwingine yeyote hapa, wakwe
zako, wana au binti, ama yeyote mwingine
aliye wako katika mji huu? Waondoe hapa,
13 [m]kwa sababu tunapaangamiza mahali
hapa. Kilio kwa BWANA dhidi ya watu wa
hapa ni kikubwa kiasi kwamba ametutuma
kupaangamiza."
14 [n]Kwa hiyo Loti alitoka ili kuzungumza
na wakwe zake, waliokuwa wamewaposa
binti zake. Akawaambia, "Fanyeni haraka
kuondoka mahali hapa, kwa kuwa BWANA
yu karibu kuangamiza mji huu!" Lakini
wakwe zake walifikiri kwamba alikuwa
akitania.
15 [o]Kunako mapambazuko, malaika
wakamhimiza Loti, wakamwambia, "Fanya
haraka! Mchukue mke wako na binti zako
wawili walioko hapa, la sivyo utaangamizwa
wakati mji utakapoadhibiwa."
16 [p]Alipositasita, wale watu wakamshika
mkono wake na mikono ya mke wake na
binti zake wawili na kuwaongoza salama
nje ya mji, kwa kuwa BWANA alikuwa
na huruma kwao. 17 [q]Mara walipokwisha
kuwatoa nje, mmoja wao akawaambia,
"Mkimbie kwa usalama wenu! Msitazame

---

[a]**18:33** Kut 31:18; Mwa 17:22; 31:55
[b]**19:1** Mwa 11:27; 17:3; 18:1, 2, 22; 48:12; Rut 2:10; 1Sam 25:23; 2Sam 14:33; 2Fal 2:15; Ebr 13:2
[c]**19:2** Mwa 18:4; Lk 7:44; Amu 19:15, 20
[d]**19:3** Mwa 18:6; 33:11; Ay 31:32; Kut 12:39
[e]**19:4** Mwa 13:13
[f]**19:5** Mwa 13:13; Law 18:22; Kum 23:18; Amu 19:22; Rum 1:24-27
[g]**19:6** Amu 19:23
[h]**19:8** Amu 19:24; 2Pet 2:7-8
[i]**19:9** Mwa 13:8; 23:4; Mdo 7:27
[j]**19:10** Mwa 18:2
[k]**19:11** Kum 28:28-29; 2Fal 6:18; Mdo 13:11
[l]**19:12** Mwa 6:18; 7:1
[m]**19:13** Kut 12:29; 2Sam 24:16; 2Fal 19:35; 1Nya 21:12, 15; 2Nya 32:21; Mwa 18:20; Za 78:49; Yer 21:12; 25:18; 44:22; 51:45
[n]**19:14** Hes 16:21; Ufu 18:4; Kut 9:21; 1Fal 13:18; Yer 5:12; 43:2; Lk 17:28
[o]**19:15** Hes 16:26; Ay 21:18; Za 58:9; 73:19; 90:5; Ufu 18:4
[p]**19:16** 2Pet 2:7; Kut 34:6; Za 33:8-9
[q]**19:17** 1Fal 19:3; Yer 48:6; Mwa 13:12; 14:10; Mt 24:16

nyuma, wala msisimame popote katika nchi
tambarare! Kimbilieni milimani, ama sivyo
mtaangamizwa!”
18 Lakini Loti akawajibu, “La hasha,
bwana zangu, tafadhalini! 19 [a]Mtumishi
wenu amepata kibali mbele ya macho
yenu, nanyi mmeonyesha wema mkubwa
kwangu kwa kuokoa maisha yangu. Lakini
siwezi kukimbilia milimani, janga hili
litanikumba, nami nitakufa. 20 Tazama,
hapa kuna mji karibu wa kukimbilia, nao
ni mdogo. Niruhusuni nikimbilie humo,
ni mdogo sana, ama sivyo? Ndipo maisha
yangu yatasalimika.”
21 [b]Akamwambia, “Vema sana,
nitalikubali hili ombi pia, sitauangamiza
mji ulioutaja. 22 [c]Lakini ukimbilie huko
haraka, kwa sababu sitaweza kufanya lolote
mpaka ufike huko.” (Ndiyo maana mji huo
ukaitwa Soari.[d])
23 [e]Wakati Loti alipofika Soari, jua
lilikuwa limechomoza katika nchi. 24 [f]Ndipo
Bwana akanyesha moto wa kiberiti uliotoka
mbinguni kwa Bwana juu ya Sodoma na
Gomora. 25 [g]Hivyo akaiteketeza miji ile na
eneo lote la tambarare, pamoja na wote
waliokuwa wanaishi katika miji, hata pia
mimea yote katika nchi. 26 [h]Lakini mke wa
Loti akatazama nyuma, hivyo akawa nguzo
ya chumvi.
27 [i]Asubuhi na mapema siku iliyofuata,
Abrahamu akaamka na kurudi mahali
pale aliposimama mbele za Bwana.
28 [j]Akatazama upande wa Sodoma na
Gomora, kuelekea nchi yote ya tambarare,
akaona moshi mzito ukipanda kutoka
kwenye nchi, kama moshi utokao kwenye
tanuru.
29 [k]Kwa hiyo Mungu alipoiangamiza miji
ya tambarare alimkumbuka Abrahamu,
akamtoa Loti kutoka kwenye lile janga
lililoharibu miji ile ambamo Loti alikuwa
ameishi.

*Loti Na Binti Zake*

30 [l]Loti na binti zake wawili waliondoka
Soari na kufanya makao yao kule milimani,
kwa maana aliogopa kukaa Soari. Yeye na
binti zake wawili waliishi katika pango.
31 Siku moja binti mkubwa akamwambia
yule mdogo, “Baba yetu ni mzee na hakuna
mwanaume mahali hapa atakayekutana na
sisi kimwili, kama ilivyo desturi ya mahali
pote duniani. 32 [m]Tumnyweshe baba yetu
mvinyo kisha tukutane naye kimwili ili
tuhifadhi uzao wetu kupitia baba yetu.”
33 Usiku ule walimnywesha baba yao
mvinyo, alipolewa binti yake mkubwa
akaingia na kukutana naye kimwili. Baba
yao hakujua wakati binti yake alipoingia
kulala naye wala alipotoka.
34 Siku iliyofuata binti mkubwa
akamwambia yule mdogo, “Usiku uliopita
mimi nilikutana kimwili na baba yangu.
Tumnyweshe divai tena, usiku huu nawe
ukutane naye kimwili ili tuweze kuhifadhi
uzao wetu kupitia baba yetu.” 35 [n]Kwa
hiyo wakamnywesha baba yao mvinyo
tena usiku ule, naye binti yake mdogo
akaingia, akakutana naye kimwili. Kwa
mara nyingine baba yao hakujua binti yake
alipolala naye wala alipoondoka.
36 Hivyo binti wawili wa Loti wakapata
mimba kwa baba yao. 37 [o]Binti mkubwa
akamzaa mwana, akamwita jina lake
Moabu; ndio baba wa Wamoabu hata leo.

---

[a]**19:19** Mwa 6:8; 18:3; 24:12; 39:21; 40:14; 47:29; Rut 1:8; 2:20; 3:10
[b]**19:21** 1Sam 25:35; 2Sam 14:8; Ay 42:9
[c]**19:22** Mwa 13:10
[d]22 Soari maana yake Mdogo.
[e]**19:23** Mwa 13:10
[f]**19:24** Ay 18:15; Za 11:6; Isa 30:33; 34:9; Eze 38:22; Kum 29:23; Isa 1:9; 13:19; Yer 49:18; 50:40; Amo 4:11; Mwa 18:17; Law 10:2; Mt 10:15; Lk 17:29; Yud 7
[g]**19:25** Eze 16:48; 26:16; Sef 3:8; Hag 2:22; Mwa 13:12; Za 107:34; Isa 1:10; Yer 20:16; 23:14; Mao 4:6
[h]**19:26** Lk 17:32
[i]**19:27** Mwa 18:22
[j]**19:28** Mwa 15:17; Kut 19:18; Ufu 9:2, 18
[k]**19:29** Mwa 8:1; 13:12; 14:12; Eze 14:16; 2Pet 2:7
[l]**19:30** Mwa 13:10; 14:10
[m]**19:32** Mwa 16:2; 38:18
[n]**19:35** Mwa 9:21
[o]**19:37** Mwa 36:35; Kut 15:15; Hes 25:1; Isa 15:1; 25:10; Yer 25:21; 48:1; Eze 25:8; Sef 2:9; Hes 22:4; 24:17; Rut 1:4, 22; 1Sam 14:47; 22:3-4; 2Sam 8:2; 2Fal 3:4; Ezr 9:1; Za 108:9

38 [a]Binti mdogo naye pia akamzaa mwana,
naye akamwita Benami; ndiye baba wa
Waamoni hata leo.

### *Abrahamu Na Abimeleki*

20 [b]Basi Abrahamu akaendelea mbele
kutoka huko hadi nchi ya Negebu na
akaishi kati ya Kadeshi na Shuri. Kwa muda
mfupi alikaa Gerari kama mgeni, 2 [c]huko
Abrahamu akasema kuhusu Sara mkewe,
“Huyu ni dada yangu.” Kisha Abimeleki
mfalme wa Gerari akatuma Sara aletwe,
naye akamchukua.
3 [d]Lakini Mungu akamjia Abimeleki katika
ndoto wakati wa usiku na kumwambia,
“Wewe ni kama mfu kwa sababu ya huyu
mwanamke uliyemchukua; yeye ni mke wa
mtu.”
4 [e]Wakati huo Abimeleki alikuwa bado
hajamsogelea, kwa hiyo akasema, “Je,
Bwana utaliharibu taifa lisilo na hatia?
5 [f]Hakusema kwangu, ‘Huyu ni dada yangu,’
naye Sara pia hakusema, ‘Huyu ni kaka
yangu’? Nimefanya haya kwa dhamiri
njema na mikono safi.”
6 [g]Kisha Mungu akamwambia katika
ndoto, “Ndiyo, najua ya kwamba
umefanya haya kwa dhamiri safi, kwa
hiyo nimekuzuia usinitende dhambi.
Ndiyo sababu sikukuacha umguse. 7 [h]Sasa
umrudishe huyo mke wa mtu, kwa maana
ni nabii, naye atakuombea nawe utaishi.
Lakini kama hutamrudisha, ujue kwa
hakika kuwa wewe na watu wako wote
mtakufa.”
8 Kesho yake asubuhi na mapema
Abimeleki akawaita maafisa wake wote,
na baada ya kuwaambia yote yaliyotokea,
waliogopa sana. 9 [i]Kisha Abimeleki
akamwita Abrahamu na kumwambia,
“Wewe umetufanyia nini? Nimekukosea
nini hata ukaleta hatia kubwa namna hii
juu yangu na ufalme wangu? Umenifanyia
mambo ambayo hayakupasa kufanyika.”
10 Abimeleki akamuuliza Abrahamu,
“Ulikuwa na kusudi gani kufanya hivi?”
11 [j]Abrahamu akajibu, “Niliwaza kwamba,
‘Hakika hakuna hofu ya Mungu mahali
hapa, nao wataniua kwa sababu ya mke
wangu.’ 12 [k]Pamoja na hayo, ni kweli
kwamba yeye ni dada yangu, binti wa baba
yangu ingawa si mtoto wa mama yangu;
basi akawa mke wangu. 13 [l]Wakati BWANA
aliponifanya nisafiri mbali na nyumbani
mwa baba yangu, nilimwambia, ‘Hivi ndivyo
utakavyoonyesha pendo lako kwangu: Kila
mahali tutakapokwenda, kuhusu mimi
sema, “Huyu ni kaka yangu.” ’ ”
14 [m]Kisha Abimeleki akatwaa kondoo
na ng’ombe, na watumwa wa kiume na
wa kike akampa Abrahamu, akamrudisha
Sara kwa mumewe. 15 [n]Abimeleki akasema,
“Nchi yangu iko mbele yako, ishi popote
unapotaka.”
16 Akamwambia Sara, “Ninampa kaka
yako shekeli elfu moja za fedha. Hii ni
kufidia kosa lililofanyika dhidi yako mbele
ya wote walio pamoja nawe; haki yako
imethibitishwa kabisa.”
17 [o]Kisha Abrahamu akamwomba Mungu,
naye Mungu akamponya Abimeleki, mke
wake, na watumwa wake wa kike kwamba

---

[a]**19:38** Hes 21:24; Kum 2:19; 23:3; Yos 12:2; Amu 3:13; 10:6-7; 1Sam 11:1-11; 14:47; 1Nya 19:1; 2Nya 20:23; 26:8; 27:5; Neh 2:19; 4:3; Yer 25:21; 40:14; 49:1; Eze 21:28; 25:2; Amo 1:13

[b]**20:1** Mwa 18:1; 12:9; 14:7; 16:7; 26:3

[c]**20:2** Mwa 12:13, 15; 26:1

[d]**20:3** Hes 12:6; 22:9, 20; Mwa 26:11; 28:12; 31:10, 24; 37:5-9; 40:5; 41:1; Kum 13:1; Kut 10:7; 12:33; Ay 33:15; Dan 2:1; 4:5; 1Nya 16:21; Za 105:14, 28

[e]**20:4** Mwa 18:25

[f]**20:5** Mwa 12:19; 17:1; Za 7:8; 25:21; 26:6; 41:12

[g]**20:6** 1Sam 25:26, 34; Mwa 13:13; Za 41:4; 51:4

[h]**20:7** Kum 18:18; 34:10; 2Fal 3:11; 5:3; 1Nya 16:22; Za 105:15; Kut 8:8; Hes 11:2; 12:13; 1Sam 7:5; 1Fal 13:6; Ay 42:8; Yer 18:20; 37:3; 42:2; Za 9:5

[i]**20:9** Mwa 12:18; 34:7

[j]**20:11** Mwa 12:12; 31:31; 42:18; Neh 5:15; Ay 31:23; Za 36:1; Mit 16:6

[k]**20:12** Mwa 12:13

[l]**20:13** Kum 26:5; 1Nya 16:20; Isa 30:28; 63:17; Mwa 12:1

[m]**20:14** Mwa 12:16

[n]**20:15** Mwa 13:9; 45:18

[o]**20:17** Ay 42:9

waweze kupata watoto tena, 18 [a]kwa kuwa
BWANA alikuwa ameyafunga matumbo ya
wote katika nyumba ya Abimeleki kwa
sababu ya Sara, mke wa Abrahamu.

*Kuzaliwa Kwa Isaki*

21 [b]Wakati huu BWANA akamrehemu
Sara kama alivyokuwa amesema, naye
BWANA akamtendea Sara kile alichokuwa
ameahidi. 2 [c]Sara akapata mimba, akamzalia
Abrahamu mwana katika uzee wake, majira
yale ya Mungu aliomwahidi. 3 [d]Abrahamu
akamwita Isaki yule mwana ambaye Sara
alimzalia. 4 [e]Isaki alipokuwa na umri wa siku
nane, Abrahamu akamtahiri, kama Mungu
alivyomwamuru. 5 [f]Abrahamu alikuwa
na miaka 100 wakati Isaki mwanawe
alipozaliwa.
6 [g]Sara akasema, "Mungu ameniletea
kicheko, kila mmoja atakayesikia jambo
hili atacheka pamoja nami." 7 [h]Akaongeza
kusema, "Nani angemwambia Abrahamu
kuwa Sara angenyonyesha watoto? Tena
nimemzalia mwana katika uzee wake."

*Hagari Na Ishmaeli Wafukuzwa*

8 [i]Mtoto akakua, akaachishwa kunyonya.
Siku hiyo Isaki alipoachishwa kunyonya,
Abrahamu alifanya sherehe kubwa.
9 [j]Lakini Sara aliona kuwa mwana ambaye
Hagari, Mmisri, aliyemzalia Abrahamu
alikuwa anadhihaki, 10 [k]Sara akamwambia
Abrahamu, "Mwondoe mwanamke huyo
mtumwa pamoja na mwanawe, kwa kuwa
mwana wa mwanamke mtumwa kamwe
hatarithi pamoja na mwanangu Isaki."
11 [l]Jambo hili lilimhuzunisha sana
Abrahamu kwa sababu lilimhusu
mwanawe. 12 [m]Lakini Mungu akamwambia,
"Usihuzunike hivyo kwa sababu ya kijana
na mtumishi wako wa kike. Sikiliza lolote
Sara analokuambia, kwa sababu uzao
wako utahesabiwa kupitia kwake Isaki.
13 [n]Nitamfanya huyu mwana wa mtumishi
wako wa kike kuwa taifa pia, kwa sababu
naye ni uzao wako."
14 [o]Kesho yake asubuhi na mapema,
Abrahamu akachukua chakula na kiriba cha
maji, akampa Hagari. Akaviweka mabegani
mwa Hagari, akamwondoa pamoja na
kijana. Hagari akashika njia, akatangatanga
katika jangwa la Beer-Sheba.
15 Maji yalipokwisha kwenye kiriba,
akamwacha kijana chini ya mojawapo ya
vichaka. 16 [p]Kisha akajiendea zake akaketi
karibu, umbali wa kutupa mshale, akawaza,
"Siwezi kumwangalia kijana akifa." Ikawa
alipokuwa ameketi pale karibu, akaanza
kulia kwa huzuni.
17 [q]Mungu akamsikia kijana akilia,
malaika wa Mungu akamwita Hagari
kutoka mbinguni na kumwambia, "Kuna
nini Hagari? Usiogope, Mungu amesikia
kijana analia akiwa amelala pale. 18 Mwinue
kijana na umshike mkono, kwa maana
nitamfanya kuwa taifa kubwa."
19 [r]Ndipo Mungu akamfumbua Hagari
macho yake naye akaona kisima cha maji.
Hivyo akaenda akajaza kiriba maji na
kumpa kijana anywe.
20 [s]Mungu akawa pamoja na huyu
kijana alipokuwa akiendelea kukua.
Aliishi jangwani na akawa mpiga upinde.
21 [t]Alipokuwa akiishi katika Jangwa la

---

[a]**20:18** Mwa 12:17
[b]**21:1** Mwa 17:20; 1Sam 2:21; Mwa 8:1; 17:6; 18:14; 4:23; Ebr 11:11
[c]**21:2** Mwa 17:19; 30:6; 18:10; Gal 4:22; Ebr 11:11
[d]**21:3** Mwa 16:11; Yos 24:3
[e]**21:4** Mwa 17:10-12; Mdo 7:8
[f]**21:5** Mwa 12:4; Ebr 6:15
[g]**21:6** Mwa 17:17; Ay 8:21; Za 126:2; Isa 12:6; 35:2; 44:23; 52:9; 54:1
[h]**21:7** Mwa 17:17
[i]**21:8** 1Sam 1:23
[j]**21:9** Mwa 16:15; 39:14; Gal 4:29
[k]**21:10** Mwa 39:17; 25:6; Gal 4:30
[l]**21:11** Mwa 17:18
[m]**21:12** Mt 1:2; Rum 9:7; Ebr 11:18
[n]**21:13** Mwa 13:16
[o]**21:14** Mwa 16:1; 22:19; 26:33; 28:10; 46:1-5; Yos 15:28; 19:2; Amu 20:1; 1Sam 3:20; 1Nya 4:28; Neh 11:27
[p]**21:16** Yer 6:26; Amo 8:10; Zek 12:10
[q]**21:17** Kut 3:7; Hes 20:16; Za 6:8; Kum 26:7; Mwa 16:7; 22:11, 15; 15:1; 17:20
[r]**21:19** Hes 22:31; Mwa 16:7
[s]**21:20** Mwa 26:3, 24; 28:15; 39:2; Lk 1:66
[t]**21:21** Mwa 14:6; 24:4, 38; 28:2; 34:4-8; Amu 14:2

Parani, mama yake akampatia mke kutoka
Misri.

*Mapatano Katika Beer-Sheba*

22 [a]Wakati huo Abimeleki na Fikoli mkuu
wa majeshi yake wakamwambia Abrahamu,
“Mungu yu pamoja nawe katika kila kitu
unachofanya. 23 [b]Sasa niapie hapa mbele
za Mungu kwamba hutanitenda hila mimi,
watoto wangu wala wazao wangu. Nitendee
mimi na nchi ambayo unaishi kama mgeni
wema ule ule ambao nimekutendea.”
24 Abrahamu akasema, “Ninaapa hivyo.”
25 [c]Ndipo Abrahamu akalalamika kwa
Abimeleki kuhusu kisima cha maji ambacho
watumishi wa Abimeleki walikuwa
wamekinyang’anya. 26 Lakini Abimeleki
akasema, “Sijui ni nani ambaye amefanya
hili. Hukuniambia, leo tu ndipo ninasikia
habari zake.”
27 [d]Hivyo Abrahamu akaleta kondoo
na ng’ombe, akampa Abimeleki, nao
watu hawa wawili wakafanya mapatano.
28 Abrahamu akatenga kondoo wa kike
saba kutoka kwenye kundi, 29 Abimeleki
akamuuliza Abrahamu, “Ni nini maana ya
hawa kondoo wa kike saba uliowatenga
peke yao?”
30 [e]Abrahamu akamjibu, “Upokee hawa
kondoo wa kike saba kutoka mkononi
mwangu kama ushahidi kuwa nilichimba
kisima hiki.”
31 Hivyo mahali pale pakaitwa Beer-
Sheba, kwa sababu watu wawili waliapiana
hapo.
32 [f]Baada ya mapatano kufanyika huko
Beer-Sheba, Abimeleki na Fikoli mkuu
wa majeshi yake wakarudi katika nchi ya
Wafilisti. 33 [g]Abrahamu akapanda mti wa
mkwaju huko Beer-Sheba, na hapo akaliitia
jina la Bwana, Mungu wa milele. 34 [h]Naye
Abrahamu akakaa katika nchi ya Wafilisti
kwa muda mrefu.

*Kujua Uthabiti Wa Abrahamu*

22 [i]Baadaye Mungu akamjaribu
Abrahamu. Akamwambia,
“Abrahamu!”

Abrahamu akajibu, “Mimi hapa.”
2 [j]Kisha Mungu akamwambia, “Umchukue
mwanao, mwana wako wa pekee, Isaki
umpendaye, uende katika nchi ya Moria.
Mtoe huko kama sadaka ya kuteketezwa juu
ya mlima mmojawapo nitakaokuambia.”
3 [k]Abrahamu akaamka asubuhi na
mapema siku iliyofuata, akamtayarisha
punda wake. Akawachukua watumishi
wake wawili pamoja na Isaki mwanawe.
Baada ya kuchanja kuni za kutosha kwa ajili
ya hiyo sadaka ya kuteketezwa, akaondoka
kuelekea mahali Mungu alipokuwa
amemwambia. 4 Siku ya tatu Abrahamu
akainua macho, akapaona mahali pale
kwa mbali. 5 [l]Akawaambia watumishi wake,
“Kaeni hapa pamoja na punda, wakati mimi
na kijana tunakwenda kule. Tutakwenda
kuabudu na kisha tutawarudia.”
6 [m]Abrahamu akachukua kuni kwa ajili
ya sadaka ya kuteketezwa, akamtwika Isaki
mwanawe, yeye mwenyewe akachukua
moto na kisu. Walipokuwa wakienda
pamoja, 7 [n]Isaki akanena akamwambia
Abrahamu baba yake, “Baba yangu!”

Abrahamu akaitika, “Mimi hapa,
mwanangu.”

---

[a]**21:22** Mwa 20:2; 26:26-28; 28:15; 31:3-5, 42; 39:2-3; Za 46:7; 1Sam 3:19; 16:18; Isa 7:14; 8:8-10; 41:10; 43:5
[b]**21:23** Mwa 25:33; 26:31; 31:53; Yos 2:12; 1Fal 2:8; 1Sam 24:21
[c]**21:25** Mwa 26:15-22
[d]**21:27** Mwa 26:28-31; 31:44, 53
[e]**21:30** Mwa 31:44-52; Isa 19:20; Yos 22:27-34; 24:27; Mal 2:14
[f]**21:32** Mwa 10:14; 26:33
[g]**21:33** 1Sam 22:6; 31:13; Mwa 4:26; Kut 15:18; Kum 32:40; 33:27; Ay 36:26; Za 10:16; 45:6; 90:2; 93:2; 102:24; 103:19; 146:10; Isa 40:28; Yer 10:10; Hab 1:12; 3:6; Ebr 13:8
[h]**21:34** Mwa 10:14
[i]**22:1** Kut 15:25; 16:4; 20:20; Kum 8:2, 16; 13:3; Amu 2:22; 3:1; 2Nya 32:31; Za 66:10; Ebr 11:17; Yak 1:12-13; Mwa 31:11; 46:2; 1Sam 3:4-8; Isa 6:8
[j]**22:2** Yn 3:16; Ebr 11:17; 1Yn 4:9; Mwa 8:20
[k]**22:3** Yos 8:10
[l]**22:5** Kut 24:14
[m]**22:6** Yn 19:17; Amu 19:29
[n]**22:7** Kut 29:38-42; Law 1:10; Ufu 13:8

Isaki akasema, “Moto na kuni zipo, Je,
yuko wapi mwana-kondoo kwa ajili ya
sadaka ya kuteketezwa?”
8 [a]Abrahamu akajibu, “Mwanangu, Mungu
mwenyewe atajipatia mwana-kondoo kwa
ajili ya hiyo sadaka ya kuteketezwa.” Nao
hawa wawili wakaendelea mbele pamoja.
9 [b]Walipofika mahali pale alipokuwa
ameambiwa na Mungu, Abrahamu
akajenga madhabahu hapo, akaziweka
kuni juu yake. Akamfunga Isaki mwanawe
na akamlaza kwenye madhabahu, juu ya
zile kuni. 10 [c]Kisha akanyoosha mkono
wake na akachukua kisu ili amchinje
mwanawe. 11 [d]Lakini malaika wa BWANA
akamwita kutoka mbinguni, akamwambia,
“Abrahamu! Abrahamu!”
Akajibu, “Mimi hapa.”
12 [e]Akamwambia, “Usimdhuru kijana,
wala usimtendee jambo lolote. Sasa ninajua
kwamba unamcha Mungu, kwa sababu
hukunizuilia mwanao, mwana wako wa
pekee.”
13 [f]Abrahamu akainua macho yake,
akaona kondoo dume amenaswa pembe
zake nyuma yake katika kichaka. Akaenda
akamchukua huyo kondoo dume, akamtoa
awe sadaka ya kuteketezwa badala ya
mwanawe. 14 [g]Abrahamu akapaita mahali
pale Yehova-Yire.[h] Mpaka siku ya leo
inasemekana, “Katika mlima wa BWANA
itapatikana.”
15 [i]Basi malaika wa BWANA akamwita
Abrahamu kutoka mbinguni mara ya pili,
16 [j]akasema, “Ninaapa kwa nafsi yangu,
asema BWANA, kwamba kwa sababu
umefanya jambo hili na hukunizuilia
mwanao, mwana wako wa pekee, 17 [k]hakika
nitakubariki, na nitauzidisha uzao wako
kama nyota za angani na kama mchanga
ulioko pwani. Wazao wako watamiliki
miji ya adui zao, 18 [l]na kupitia uzao wako
mataifa yote duniani yatabarikiwa, kwa
sababu umenitii.”
19 [m]Ndipo Abrahamu akawarudia
watumishi wake, wakaondoka wakaenda
wote pamoja mpaka Beer-Sheba. Abrahamu
akaishi huko Beer-Sheba.

*Wana Wa Nahori*

20 [n]Baada ya muda, Abrahamu
akaambiwa, “Milka pia amepata watoto,
amemzalia ndugu yako Nahori wana: 21 [o]Usi
mzaliwa wake wa kwanza, Buzi nduguye,
Kemueli (baba wa Aramu), 22 [p]Kesedi, Hazo,
Pildashi, Yidlafu na Bethueli.” 23 [q]Bethueli
akamzaa Rebeka. Milka alimzalia Nahori
nduguye Abrahamu hao wana wanane.
24 [r]Suria wake Nahori aliyeitwa Reuma pia
alikuwa na wana: Teba, Gahamu, Tahashi
na Maaka.

*Kifo Cha Sara*

23 Sara aliishi akawa na umri wa miaka
mia na ishirini na saba. 2 [s]Sara
akafa huko Kiriath-Arba (yaani Hebroni)
katika nchi ya Kanaani, Abrahamu
akamwombolezea na kumlilia Sara.
3 [t]Ndipo Abrahamu akainuka kutoka pale
penye maiti ya mke wake. Akazungumza

---

[a]**22:8** Yn 1:29
[b]**22:9** Mwa 4:26; 8:20; Law 1:7; 1Fal 18:33; Ebr 11:17-19; Yak 2:21
[c]**22:10** Mwa 18:19
[d]**22:11** Mwa 16:7; 21:17; 46:2
[e]**22:12** Mwa 18:19; 42:18; Kut 18:21; 1Sam 15:22; Ay 1:1; 37:24; Mit 8:13; Yak 2:21-23; Yn 3:16; 1Yn 4:9
[f]**22:13** Mwa 8:20; Rum 8:32
[g]**22:14** Kut 17:15; Amu 6:24; Isa 30:29
[h]14 Yehova-Yire maana yake BWANA atatupa.
[i]**22:15** Mwa 21:17
[j]**22:16** Kut 13:11; 32:13; 33:1; Isa 45:23; 62:8; Yer 22:5; 44:26; 49:13; 51:14; Amo 6:8; Ebr 6:13; Lk 1:73
[k]**22:17** Mwa 12:2; 15:5; 26:24; 24:60; Ebr 6:14; Kut 32:13; Kum 7:7; 28:62; Hos 1:10; Rum 9:27; Ebr 11:12; Es 9:2
[l]**22:18** Mwa 12:2-3; 17:2, 9; Mdo 3:25; Gal 3:8; Za 105:9
[m]**22:19** Mwa 21:14; 26:23; 28:10
[n]**22:20** Mwa 11:29
[o]**22:21** Mwa 10:23; Ay 32:2; Yer 25:23
[p]**22:22** Mwa 24:15, 47; 25:20
[q]**22:23** Mwa 24:15; 11:29
[r]**22:24** Mwa 25:6; 35:22; 36:12; Amu 8:31; 2Sam 3:7; 1Fal 2:22; 11:3; 1Nya 1:32; Wim 6:8
[s]**23:2** Yos 14:15; 15:13; 20:7; 21:11; Mwa 13:18; 24:67
[t]**23:3** Mwa 10:15

na Wahiti, akasema, 4 [a]“Mimi ni mpitaji na
mgeni miongoni mwenu. Niuzieni sehemu
ya ardhi yenu ili niweze kumzika maiti
wangu.”
5 Wahiti wakamjibu Abrahamu,
6 [b]“Bwana, tusikilize. Wewe ni mtawala
mkuu sana miongoni mwetu. Zika maiti
wako katika kaburi unalolipenda kati ya
makaburi yetu. Hakuna mtu wa kwetu
atakayekuzuia kaburi lake ili kuzika maiti
wako.”
7 Abrahamu akainuka na akasujudu
mbele ya wenyeji wa nchi, yaani Wahiti.
8 Akawaambia, “Kama mnaniruhusu
kumzika maiti wangu, basi nisikilizeni
mkamsihi Efroni mwana wa Sohari kwa
niaba yangu 9 [c]ili aniuzie pango la Makpela,
lililo mali yake, nalo liko mwisho wa
shamba lake. Mwambieni aniuzie kwa bei
kamili atakayosema ili liwe mahali pangu
pa kuzikia miongoni mwenu.”
10 [d]Efroni Mhiti alikuwa ameketi miongoni
mwa watu wake, akamjibu Abrahamu
mbele ya Wahiti wote waliokuwepo katika
lango la mji. 11 [e]“La hasha, bwana wangu,
nisikilize, nakupa shamba, pia nakupa
pango lililomo ndani yake. Nakupa mbele
ya watu wangu. Uzike maiti wako.”
12 Abrahamu akasujudu tena, mbele ya
wenyeji wa nchi, 13 akamwambia Efroni
wale watu wakiwa wanasikia, “Tafadhali
nisikilize. Nitakulipa fedha za hilo shamba.
Kubali kuzipokea ili niweze kumzika maiti
wangu.”
14 Efroni akamjibu Abrahamu,
15 [f]“Nisikilize, bwana wangu, thamani ya
ardhi hiyo ni shekeli 400 za fedha,[g] lakini
hiyo ni nini kati yako na mimi? Mzike maiti
wako.”
16 [h]Abrahamu akakubali masharti ya
Efroni, akampimia ile fedha aliyotaja
masikioni mwa Wahiti: Shekeli 400 za
fedha kulingana na viwango vya uzito
vilivyokuwa vikitumika wakati huo na
wafanyabiashara.
17 [i]Hivyo shamba la Efroni huko Makpela
karibu na Mamre, yaani shamba pamoja
na pango lililokuwamo, nayo miti yote
iliyokuwamo ndani ya mipaka ya shamba
hilo, vilikabidhiwa, 18 [j]kwa Abrahamu
kuwa mali yake mbele ya Wahiti wote
waliokuwa wamekuja kwenye lango la mji.
19 [k]Baada ya hayo Abrahamu akamzika Sara
mkewe kwenye pango ndani ya shamba la
Makpela karibu na Mamre (huko Hebroni)
katika nchi ya Kanaani. 20 Hivyo Wahiti
wakamkabidhi Abrahamu shamba pamoja
na pango lililokuwa humo kuwa mahali
pa kuzikia.

### *Isaki Na Rebeka*

24 [l]Wakati huu Abrahamu alikuwa
mzee mwenye miaka mingi, naye
BWANA alikuwa amembariki katika kila
njia. 2 [m]Akamwambia mtumishi wake
mkuu wa vitu vyote katika nyumba yake,
yule aliyekuwa msimamizi wa vitu vyote
alivyokuwa navyo, “Weka mkono wako
chini ya paja langu, 3 [n]Ninataka uape kwa
BWANA, Mungu wa mbingu na Mungu wa
nchi, kwamba hutamtwalia mwanangu mke
kutoka binti za Wakanaani, ambao ninaishi
miongoni mwao, 4 [o]bali utakwenda katika
nchi yangu na jamaa zangu umpatie Isaki
mwanangu mke.”
5 [p]Yule mtumishi akamuuliza, “Je, kama

[a]**23:4** Mwa 17:8; 19:9; 49:30; Kut 2:22; Law 25:23; Za 39:12; 105:12; 119:19; Ebr 11:9-13; Mdo 7:16
[b]**23:6** Mwa 14:14-16; 24:35; 25:9
[c]**23:9** Mwa 25:9; 47:30; 49:30; 50:13
[d]**23:10** Kum 22:15; 25:7; Yos 20:4; Rut 4:11; 2Sam 15:2; 2Fal 15:35; Za 127:5; Mit 31:23; Yer 26:10; 6:10
[e]**23:11** 2Sam 24:23
[f]**23:15** Eze 45:12
[g]15 Shekeli 400 za fedha ni sawa na kilo 4.5.
[h]**23:16** 2Sam 14:26; 24:24; Yer 32:9; Zek 11:12
[i]**23:17** Mwa 13:18
[j]**23:18** Mwa 18:1, 7
[k]**23:19** Mwa 13:18; Yos 14:13; 1Nya 29:27; 23:20; Yer 32:10; Mwa 10:15; 35:29; 49:30, 31; 50:5
[l]**24:1** Mwa 17:17; Yos 23:1; Mwa 12:2; Gal 3:9
[m]**24:2** Mwa 15:3; 39:4-6; 47:29
[n]**24:3** Mwa 10:15-19; 47:31; 50:25; 14:19; Hes 20:14; 2Kor 6:14-17
[o]**24:4** Mwa 12:1; 21:21; Amu 14:3
[p]**24:5** Ebr 11:15

huyo mwanamke atakataa kuja nami katika
nchi hii? Je, nimpeleke mwanao katika hiyo
nchi uliyotoka?”
6 Abrahamu akasema, “Hakikisha
kwamba hutamrudisha mwanangu huko.
7 [a]BWANA, Mungu wa mbingu, aliyenitoa
nyumbani kwa baba yangu na nchi
yangu niliyozaliwa na aliyesema nami na
akaniahidi kwa kiapo, akisema, ‘Nitawapa
watoto wako nchi hii,’ atatuma malaika
wake akutangulie ili umpatie mwanangu
mke kutoka huko. 8 [b]Kama huyo mwanamke
asipokubali kufuatana nawe, basi
utafunguliwa kutoka kiapo nilichokuapisha.
Ila usimrudishe mwanangu huko.” 9 [c]Basi
yule mtumishi akaweka mkono wake
chini ya paja la bwana wake Abrahamu
akamwapia kuhusu shauri hili.
10 [d]Ndipo huyo mtumishi akachukua
ngamia kumi miongoni mwa ngamia za
bwana wake, akaondoka, akiwa amechukua
aina zote za vitu vizuri kutoka kwa bwana
wake. Akaelekea Aramu-Naharaimu[e]
na kushika njia kwenda mji wa Nahori.
11 [f]Akawapigisha ngamia magoti karibu
na kisima cha maji nje ya mji, ilikuwa
inaelekea jioni, wakati ambapo wanawake
wanakuja kuteka maji.
12 [g]Kisha akaomba, “Ee BWANA, Mungu
wa bwana wangu Abrahamu, nipatie
ushindi leo, uonyeshe huruma kwa bwana
wangu Abrahamu. 13 Tazama, nimesimama
karibu na kisima hiki cha maji, nao binti
za watu wa mji huu wanakuja kuteka maji.
14 [h]Basi na iwe hivi, nitakapomwambia
binti mmojawapo, ‘Tafadhali tua mtungi
wako nipate kunywa maji,’ naye akisema,
‘Kunywa, nitawanywesha na ngamia wako
pia.’ Basi na awe ndiye uliyemchagua kwa
ajili ya mtumishi wako Isaki. Kwa hili
nitajua umemhurumia bwana wangu.”
15 [i]Ikawa kabla hajamaliza kuomba,
Rebeka akatokea akiwa na mtungi begani
mwake. Alikuwa binti wa Bethueli. Bethueli
alikuwa mwana wa Milka aliyekuwa mke
wa Nahori ndugu wa Abrahamu. 16 [j]Huyu
msichana alikuwa mzuri sana wa sura,
bikira, ambaye hakuna mtu aliyekuwa
amekutana naye kimwili. Aliteremka
kisimani, akajaza mtungi wake akapanda
juu.
17 [k]Ndipo yule mtumishi akaharakisha
kukutana naye akamwambia, “Tafadhali
nipe maji kidogo katika mtungi wako.”
18 Yule msichana akasema, “Kunywa,
bwana wangu.” Akashusha kwa haraka
mtungi mkononi mwake na akampa,
akanywa.
19 Baada ya kumpa yule mtumishi yale
maji, akamwambia, “Nitateka maji kwa
ajili ya ngamia zako pia mpaka wote
watosheke.” 20 Akafanya haraka kumimina
maji kwenye birika ya kunywesheа
wanyama, akakimbia kisimani kuteka maji
mengine na akateka ya kuwatosha ngamia
wake wote. 21 Pasipo kusema neno, yule
mtumishi akamtazama kwa makini aone
kama BWANA ameifanikisha safari yake,
au la.
22 [l]Ikawa ngamia walipokwisha kunywa
wote, yule mtumishi akampa huyo
msichana pete ya puani ya dhahabu yenye
uzito wa beka moja[m] na bangili mbili za
dhahabu zenye uzito wa shekeli kumi.[n]
23 [o]Kisha akamuuliza, “Wewe ni binti wa
nani? Tafadhali uniambie, je, kuna nafasi

[a]**24:7** Mwa 12:1, 7; 16:7; Rum 4:15; Gal 3:16
[b]**24:8** Yos 2:12-20; 9:20
[c]**24:9** Mwa 32:4; 33:8
[d]**24:10** 1Fal 10:2; 1Nya 12:40; Isa 30:6; Mwa 11:29; 43:11; 45:25; Hes 23:7; Kum 23:4; Amu 3:8
[e]10 Yaani Mesopotamia ya Kaskazini-Magharibi.
[f]**24:11** Kut 2:15-16; 1Sam 9:11; Yn 4:7; Mwa 29:2, 9-10
[g]**24:12** Mwa 19:19; 26:24; 27:20; 28:13; 31:42, 53; 32:9; 43:23; 46:3; Kut 3:6; 1Fal 18:36; Za 75:9; 94:7; Neh 1:11; Yos 2:12; Ay 10:12
[h]**24:14** Amu 6:17, 37; 1Sam 14:10; 1Fal 13:3; Za 86:17; Isa 38:7; Yer 44:29
[i]**24:15** Mwa 22:22-23; 11:29
[j]**24:16** Mwa 12:11; Kum 22:15-21
[k]**24:17** 1Fal 17:10; Yn 4:7
[l]**24:22** Mwa 41:42; Isa 3:21; Eze 16:11-12
[m]22 Beka moja ya dhahabu ni sawa na gramu 5.5.
[n]22 Shekeli 10 za dhahabu ni sawa na gramu 110.
[o]**24:23** Amu 19:15; 20:4

katika nyumba ya baba yako tutakapoweza
kulala?”
24 [a]Yule msichana akamjibu, “Mimi ni binti
wa Bethueli, mwana wa Milka aliyemzalia
Nahori.” 25 [b]Akaendelea kusema, “Kwetu
kuna majani mengi na malisho, tena kuna
nafasi kwa ajili yenu kulala.”
26 [c]Yule mtumishi akasujudu na
kumwabudu BWANA, 27 [d]akisema,
“Atukuzwe BWANA, Mungu wa bwana
wangu Abrahamu, ambaye hakuondoa
wema na uaminifu wake kwa bwana
wangu. Mimi nami, BWANA ameniongoza
safarini akanifikisha nyumbani kwa jamaa
za bwana wangu.”
28 [e]Yule msichana akakimbia akawaeleza
watu wa nyumbani mwa mama yake
kuhusu mambo haya. 29 [f]Rebeka alikuwa na
kaka aliyeitwa Labani, huyo akaharakisha
kukutana na yule mtumishi kule kisimani.
30 [g]Mara alipoiona ile pete puani, na
bangili mikononi mwa dada yake na
kusikia yale maneno Rebeka aliyoambiwa
na huyo mtumishi, alimwendea huyo
mtumishi, akamkuta amesimama karibu
na ngamia wake pale karibu na kisima.
31 [h]Akamwambia, “Karibu nyumbani
wewe uliyebarikiwa na BWANA, kwa nini
unasimama huko nje? Mimi nimekuandalia
nyumba na mahali kwa ajili ya ngamia.”
32 [i]Hivyo yule mtumishi akaenda
nyumbani, mizigo ikaondolewa juu ya
ngamia. Majani na malisho yakaletwa
kwa ajili ya ngamia na maji kwa ajili yake
na watu wake ili kunawa miguu. 33 Ndipo
chakula kikaandaliwa kwa ajili yake,
lakini akasema, “Sitakula mpaka niwe
nimewaambia yale niliyo nayo ya kusema.”
Labani akasema, “Basi tuambie.”
34 [j]Hivyo akasema, “Mimi ni mtumishi
wa Abrahamu. 35 [k]BWANA amembariki sana
bwana wangu, amekuwa tajiri. Amempa
kondoo na ng’ombe, fedha na dhahabu,
watumishi wa kiume na wa kike, ngamia
na punda. 36 [l]Sara mkewe bwana wangu
amemzalia mwana katika uzee wake,
naye amempa kila kitu alichokuwa nacho.
37 [m]Naye bwana wangu ameniapisha na
akasema, ‘Kamwe usimtwalie mwanangu
mke katika binti za Wakanaani, ambao
ninaishi katika nchi yao, 38 [n]ila uende
mpaka kwa jamaa ya baba yangu na ukoo
wangu mwenyewe, ukamtwalie mwanangu
mke huko.’
39 “Kisha nikamuuliza bwana wangu, ‘Je,
kama huyo mwanamke hatakubali kurudi
nami?’
40 [o]“Akanijibu, ‘BWANA ambaye
nimetembea mbele zake, atatuma malaika
wake pamoja nawe, na kuifanikisha
safari yako, ili uweze kupata mke kwa
ajili ya mwanangu katika ukoo wangu
na kutoka jamaa ya baba yangu. 41 Kisha,
utakapokwenda kwenye ukoo wangu,
utakuwa umefunguliwa kutoka kiapo
changu hata kama wakikataa kukupa huyo
binti, utakuwa umefunguliwa kutoka kiapo
changu.’
42 “Nilipokuja kisimani leo nilisema,
‘Ee BWANA, Mungu wa bwana wangu
Abrahamu, ikikupendeza, naomba
uifanikishe safari niliyoijia. 43 [p]Tazama,
ninasimama kando ya kisima hiki, kama
mwanamwali akija kuteka maji nami
nikimwambia, tafadhali niruhusu ninywe
maji kidogo kutoka kwenye mtungi wako,
44 naye kama akiniambia, “Kunywa, nami
nitateka maji kwa ajili ya ngamia wako
pia,” basi huyo awe ndiye mke ambaye
BWANA amemchagulia mwana wa bwana
wangu.’

[a]**24:24** Mwa 11:29
[b]**24:25** Amu 19:19
[c]**24:26** Kut 4:31; 12:27; 1Nya 29:20; 2Nya 20:18
[d]**24:27** Mwa 14:20; 32:10; 47:29; Kut 18:20; Rut 4:14; 1Sam 25:32; 2Sam 18:28; 1Fal 8:56; Za 28:6; 41:13; 68:19; 98:3; 106:48; Yos 2:14; Lk 1:68
[e]**24:28** Mwa 29:12
[f]**24:29** Mwa 25:20; 27:43; 28:2-5; 29:5, 12-13
[g]**24:30** Eze 23:42
[h]**24:31** Mwa 26:29; Rut 3:10; Za 115:15
[i]**24:32** Mwa 18:4; Amu 19:21
[j]**24:34** Mwa 15:3
[k]**24:35** Mwa 12:2, 16; 23:6
[l]**24:36** Mwa 17:17; 25:5; 26:14
[m]**24:37** Mwa 50:5
[n]**24:38** Mwa 21:21
[o]**24:40** Mwa 5:22; 12:1; 16:7
[p]**24:43** Mit 30:19; Isa 7:14

45 [a]“Kabla sijamaliza kuomba moyoni
mwangu, Rebeka akatokea, amebeba mtungi
begani mwake. Akashuka kisimani akateka
maji, nami nikamwambia, ‘Tafadhali nipe
maji ninywe.’
46 “Akafanya haraka kushusha mtungi
wake begani na kusema, ‘Kunywa na
nitawanywesha ngamia wako pia,’ basi
nikanywa, akawanywesha na ngamia pia.
47 [b]“Nikamuuliza, ‘Wewe ni binti wa
nani?’

“Akasema, ‘Mimi ni binti wa Bethueli,
mwana wa Nahori, Milka aliyemzalia.’

“Ndipo nilipotia pete puani mwake na
bangili mikononi mwake, 48 nikasujudu
na nikamwabudu BWANA. Nikamtukuza
BWANA, Mungu wa bwana wangu
Abrahamu, aliyeniongoza katika njia sahihi
ili nimtwalie mwana na bwana wangu mke
katika jamaa zake. 49 Ikiwa mtaonyesha
wema na uaminifu kwa bwana wangu,
mniambie, la sivyo, mniambie, ili niweze
kujua njia ya kugeukia.”
50 [c]Labani na Bethueli wakajibu, “Jambo
hili limetoka kwa BWANA, hatuwezi
kukuambia jambo lolote baya au jema.
51 Rebeka yuko hapa, mchukue na uende,
awe mke wa mwana wa bwana wako,
sawasawa na BWANA alivyoongoza.”
52 Ikawa huyo mtumishi wa Abrahamu
aliposikia waliyosema, alisujudu mpaka
nchi mbele za BWANA. 53 [d]Ndipo huyo
mtumishi akatoa vitu vilivyotengenezwa
kwa dhahabu na kwa fedha pamoja na
mavazi, akampa Rebeka, pia akawapa
zawadi za thamani kubwa nduguye na
mamaye. 54 [e]Kisha yeye na wale watu
waliokuwa pamoja naye wakala, wakanywa
na kulala palepale.

Walipoamka asubuhi, yule mtumishi,
akasema, “Nipeni ruhusa nirudi kwa bwana
wangu.”
55 [f]Lakini ndugu yake Rebeka pamoja
na mama yake wakajibu, “Acha binti
akae kwetu siku kumi au zaidi, ndipo
mwondoke.”
56 Lakini yule mtumishi akawaambia,
“Msinicheleweshe, kwa kuwa BWANA
amefanikisha safari yangu, nipeni ruhusa
nirudi kwa bwana wangu.”
57 Ndipo wakasema, “Acha tumwite huyo
binti tumuulize, tusikie atakavyosema.”
58 [g]Kwa hiyo wakamwita Rebeka na
kumuuliza, “Je, utakwenda na mtu huyu?”

Akasema, “Nitakwenda.”
59 [h]Hivyo wakamwaga ndugu yao
Rebeka aondoke, pamoja na mjakazi wake,
mtumishi wa Abrahamu na watu wake.
60 [i]Wakambariki Rebeka, wakamwambia,

“Ndugu yetu, uwe wewe kumi elfu,
mara elfu nyingi,
nao wazao wako wamiliki
malango ya adui zao.”

61 [j]Rebeka na vijakazi wake wakajiandaa,
wakapanda ngamia zao wakafuatana na
yule mtu. Hivyo yule mtumishi akamchukua
Rebeka akaondoka.
62 [k]Basi Isaki alikuwa ametoka Beer-Lahai-
Roi, kwa kuwa alikuwa anaishi nchi ya
Negebu. 63 [l]Isaki akatoka kwenda shambani
kutafakari wakati wa jioni, alipoinua macho
yake, akaona ngamia wanakuja. 64 [m]Rebeka
pia akainua macho akamwona Isaki.
Akashuka kutoka kwenye ngamia wake
65 [n]na akamuuliza yule mtumishi, “Ni nani
mtu yule aliye kule shambani anayekuja
kutulaki?”

Yule mtumishi akajibu, “Huyu ndiye
bwana wangu.” Hivyo Rebeka akachukua
shela yake akajifunika.
66 Kisha yule mtumishi akamweleza Isaki

---

[a]**24:45** 1Sam 1:13; Yn 4:7
[b]**24:47** Mwa 22:22; Isa 3:19; Eze 16:11-12
[c]**24:50** Za 118:23; Mwa 22:22; 31:24-29; 48:16
[d]**24:53** Mwa 45:22; Kut 3:22; 12:35; 2Fal 5:5
[e]**24:54** Mwa 30:25
[f]**24:55** Amu 19:3-4
[g]**24:58** Rum 1:16
[h]**24:59** Mwa 35:8
[i]**24:60** Mwa 17:16; 22:17; 27:4; 31:55; 48:9, 15, 20; Yos 22:6; Mit 27:11
[j]**24:61** Mwa 16:1; 30:3; 46:25
[k]**24:62** Mwa 16:14; 12:9
[l]**24:63** Za 77:12; 119:15, 27; 143:5; 145:5; Mwa 18:2
[m]**24:64** Mwa 31:17, 34; 1Sam 30:17
[n]**24:65** Mwa 38:14; Wim 4:1-3; 6:7; Isa 47:2

mambo yote aliyoyatenda. 67 [a]Ndipo Isaki
akamwingiza Rebeka katika hema la Sara
mama yake, Isaki akamchukua Rebeka,
hivyo akawa mke wake. Isaki akampenda,
akafarijika baada ya kifo cha mama yake.

*Kifo Cha Abrahamu*

25 Abrahamu alioa mke mwingine,
ambaye jina lake aliitwa Ketura.
2 [b]Huyu alimzalia Zimrani, Yokshani,
Medani, Midiani, Ishbaki na Shua.
3 Yokshani alikuwa baba wa Sheba na
Dedani, wazao wa Dedani walikuwa
Waashuri, Waletushi na Waleumi. 4 [c]Wana
wa Midiani walikuwa Efa, Eferi, Hanoki,
Abida na Eldaa. Hawa wote walikuwa uzao
wa Ketura.

5 [d]Abrahamu akamwachia Isaki kila kitu
alichokuwa nacho. 6 [e]Lakini Abrahamu
alipokuwa bado hai, akawapa watoto wa
masuria wake zawadi, kisha akawaondoa
waende kuishi pande za mashariki mbali
na mwanawe Isaki.

7 [f]Kwa jumla, Abrahamu aliishi miaka
175. 8 [g]Ndipo Abrahamu akapumua
pumzi ya mwisho na akafa akiwa
mwenye umri mzuri, mzee aliyeshiba
siku, naye akakusanywa pamoja na watu
wake. 9 [h]Watoto wake Isaki na Ishmaeli
wakamzika katika pango la Makpela karibu
na Mamre, katika shamba lililokuwa la
Efroni mwana wa Sohari Mhiti, 10 [i]Shamba
ambalo Abrahamu alilinunua kwa Wahiti.
Hapo ndipo Abrahamu alipozikwa pamoja
na mkewe Sara. 11 [j]Baada ya kifo cha
Abrahamu, Mungu akambariki mwanawe
Isaki, ambaye baadaye aliishi karibu na
Beer-Lahai-Roi.

*Wana Wa Ishmaeli*

12 [k]Hivi ndivyo vizazi vya Ishmaeli mtoto
wa Abrahamu, ambaye mjakazi wake Sara,
Hagari Mmisri, alimzalia Abrahamu.

13 [l]Haya ndiyo majina ya wana wa
Ishmaeli, yaliyoorodheshwa kulingana na
jinsi walivyozaliwa: Mzaliwa wa kwanza
wa Ishmaeli ni Nebayothi, akafuatia
Kedari, Adbeeli, Mibsamu, 14 [m]Mishma,
Duma, Masa, 15 [n]Hadadi, Tema, Yeturi,
Nafishi na Kedema. 16 [o]Hawa walikuwa
wana wa Ishmaeli na haya ni majina ya
viongozi wa makabila kumi na mawili
kulingana na makao yao na kambi zao.
17 Kwa jumla Ishmaeli aliishi miaka 137.
Akapumua pumzi ya mwisho, akafa, naye
akakusanywa pamoja na watu wake.
18 [p]Wazao wa Ishmaeli waliishi kuanzia nchi
ya Havila hadi Shuri, karibu na mpaka wa
Misri, unapoelekea Ashuru. Hao waliishi
kwa uhasama na ndugu zao wote.

*Yakobo Na Esau*

19 Hivi ndivyo vizazi vya Isaki mwana
wa Abrahamu.

Abrahamu akamzaa Isaki, 20 [q]Isaki alikuwa
na umri wa miaka arobaini alipomwoa
Rebeka binti Bethueli Mwaramu kutoka
Padan-Aramu, nduguye Labani Mwaramu.

21 [r]Isaki akamwomba BWANA kwa
ajili ya mke wake, kwa sababu alikuwa

[a]**24:67** Mwa 31:33; 18:9; 25:20; 49:31; 29:18-20; 23:1-2; 34:3; Amu 16:4
[b]**25:2** Yer 25:25; Mwa 36:35; 37:28, 36; Kut 2:15; Hes 22:4; 25:6; Amu 6:1-3; 8:22-24; 9:17; Za 83:9; Isa 9:4; 10:26; Hab 3:7; Ay 2:11
[c]**25:4** Isa 60:6
[d]**25:5** Mwa 24:36
[e]**25:6** Mwa 22:24; 21:10; Amu 6:3, 33; 1Fal 4:30; Eze 25:4
[f]**25:7** Mwa 12:4; 35:28; 47:9, 28; 50:22; Ay 42:16
[g]**25:8** Mwa 35:29; 49:29; Hes 20:24; 31:2; Kum 31:14; 32:50; 34:5
[h]**25:9** Mwa 35:29; 47:30; 49:31; 23:9; 13:18; 50:13
[i]**25:10** Mwa 10:15
[j]**25:11** Mwa 12:2; 16:14
[k]**25:12** Mwa 2:4; 17:20; 21:18
[l]**25:13** Mwa 28:9; 36:3; Za 120:5; Isa 21:16; 42:11; 60:7; Yer 2:10; 49:28; Eze 27:21
[m]**25:14** Yos 15:25; Oba 1:1; Isa 21:11
[n]**25:15** Ay 6:19; Isa 21:14; Yer 25:23; 1Nya 5:19
[o]**25:16** Mwa 17:20; 13:16; Za 83:9
[p]**25:18** Mwa 17:20; 21:18; 16:7, 12
[q]**25:20** Mwa 26:34; 48:7; 35:28; 24:67; 22:22; 28:2-6; 30:20; 31:18; 33:18; 46:15; 24:29; Kum 26:5
[r]**25:21** Mwa 30:17, 22; 11:30; Ezr 8:23; 1Sam 1:17, 23; 1Nya 5:20; 2Nya 33:13; Za 127:3

tasa. BWANA akajibu maombi yake na
Rebeka mkewe akapata mimba. 22 [a]Watoto
wakashindana tumboni mwake, akasema,
“Kwa nini haya yanatokea kwangu?” Kwa
hiyo akaenda kumuuliza BWANA.
23 BWANA akamjibu,

“Mataifa mawili yamo tumboni
mwako,
na mataifa hayo mawili
kutoka ndani yako
watatenganishwa.
Mmoja atakuwa na nguvu zaidi
kuliko mwingine,
na yule mkubwa atamtumikia yule
mdogo.”

24 Wakati wake wa kujifungua ulipotimia,
walikuwepo mapacha wa kiume tumboni
mwake. 25 Wa kwanza kuzaliwa alikuwa
mwekundu, mwili wake wote ulikuwa kama
mtu aliyevaa vazi lenye nywele; wakamwita
jina lake Esau.[b] 26 Baadaye, ndugu yake
akatoka, mkono wake ukiwa umemshika
Esau kisigino; akaitwa jina lake Yakobo.[c]
Isaki alikuwa mwenye miaka sitini Rebeka
alipowazaa.
27 Watoto wakakua, naye Esau akakuwa
mwindaji hodari, mtu wa mbugani, wakati
Yakobo alikuwa mtu mtulivu, mwenye
kukaa nyumbani. 28 Isaki, ambaye alikuwa
anapendelea zaidi nyama za porini,
alimpenda Esau, bali Rebeka alimpenda
Yakobo.
29 Siku moja Yakobo alipika mchuzi wa
dengu, Esau akarudi kutoka porini akiwa
na njaa kali. 30 Esau akamwambia Yakobo,
“Haraka, nipe huo mchuzi mwekundu!
Nina njaa kali sana!” (Hii ndiyo sababu
pia aliitwa Edomu.)[d]
31 Yakobo akamjibu, “Niuzie kwanza haki
yako ya mzaliwa wa kwanza.”
32 Esau akasema, “Tazama, mimi niko
karibu ya kufa, itanifaa nini haki ya
mzaliwa wa kwanza?”
33 Yakobo akamwambia, “Niapie kwanza.”
Hivyo Esau akamwapia, akamuuzia Yakobo
haki yake ya kuzaliwa.
34 Ndipo Yakobo akampa Esau mkate na
ule mchuzi wa dengu. Akala na kunywa,
kisha akainuka akaenda zake.
Kwa hiyo Esau alidharau haki yake ya
mzaliwa wa kwanza.

*Isaki Na Abimeleki*

26 [e]Basi njaa kubwa ikawa katika nchi
hiyo, kuliko ile njaa iliyotangulia
iliyotokea wakati wa Abrahamu. Isaki
akamwendea Abimeleki mfalme wa
Wafilisti huko Gerari. 2 [f]BWANA akamtokea
Isaki, akamwambia, “Usiende Misri, bali
ukae katika nchi nitakayokuambia. 3 [g]Kaa
katika nchi hii kwa kitambo, mimi nitakuwa
pamoja na wewe na nitakubariki. Kwa
maana nitakupa wewe na uzao wako nchi
hizi zote na nitatimiza kiapo nilichomwapia
Abrahamu baba yako. 4 [h]Nitafanya wazao
wako kuwa wengi kama nyota za angani,
nami nitawapa nchi hizi zote na kutokana
na uzao wako mataifa yote yatabarikiwa,
5 [i]kwa sababu Abrahamu alinitii mimi
akatunza kanuni zangu na maagizo yangu,
amri zangu pamoja na sheria zangu.”
6 [j]Hivyo Isaki akaishi huko Gerari.
7 [k]Watu wa mahali pale walipomuuliza
habari za mke wake, akasema, “Huyu ni
dada yangu,” kwa sababu aliogopa kusema,
“Huyu ni mke wangu.” Alifikiri, “Watu wa
mahali pale wataweza kumuua kwa sababu
ya Rebeka, kwa kuwa alikuwa mzuri wa
sura.”
8 Wakati Isaki alipokuwa amekaa huko
siku nyingi, Abimeleki mfalme wa Wafilisti
akachungulia dirishani, akaona jinsi Isaki
alivyomkumbatia Rebeka mke wake.

---

[a]**25:22** Kut 18:15; 28:30; 33:7; Law 24:12; Hes 9:6-8; 27:5; Kum 17:9; 2Fal 3:11; 22:13; Isa 30:2; Yer 21:2; 37:7; Eze 14:7; 2
[b]25 Esau maana yake Mwenye nywele nyingi.
[c]26 Yakobo maana yake Ashikaye kisigino, au Atwaaye mahali pa mwingine, au Mdanganyaji, au Mwenye hila, au Mlaghai, au Mjanja.
[d]30 Edomu maana yake Mwekundu.

[e]**26:1** Mwa 12:10; 20:1
[f]**26:2** Mwa 12:1, 7; 46:3
[g]**26:3** Kut 3:12; Mwa 12:2, 7
[h]**26:4** Mwa 26:24; 48:4; 12:2
[i]**26:5** Mwa 18:19; Za 119:80, 112; Eze 18:21
[j]**26:6** Mwa 20:1
[k]**26:7** Mwa 12:13

9 Abimeleki akamwita Isaki akamwambia,
“Hakika huyu ni mke wako! Mbona
uliniambia, ‘Huyu ni dada yangu?’ ”
Isaki akamjibu, “Kwa sababu nilifikiri
ningeweza kuuawa kwa sababu yake.”
10 [a]Ndipo Abimeleki akamjibu, “Ni nini
hiki ulichotufanyia? Ingewezekana mtu
yeyote akawa amekutana kimwili na mke
wako, nawe ungeleta hatia juu yetu.”
11 [b]Hivyo Abimeleki akatoa amri kwa watu
wote, akisema, “Yeyote atakayemnyanyasa
mtu huyu au mkewe hakika atauawa.”
12 [c]Isaki akapanda mazao katika nchi
hiyo, kwa mwaka huo huo, akavuna mara
mia, kwa sababu Bwana alimbariki.
13 [d]Isaki akawa tajiri, mali zake zikaendelea
kuongezeka mpaka akawa tajiri sana.
14 [e]Akawa na mifugo ya kondoo na ng’ombe,
na watumishi wengi sana, kiasi kwamba
Wafilisti wakamwonea wivu. 15 [f]Kwa hiyo
visima vyote vilivyochimbwa na watumishi
wakati wa Abrahamu baba yake, Wafilisti
wakavifukia, wakavijaza udongo.
16 Ndipo Abimeleki akamwambia Isaki,
“Ondoka kwetu, kwa maana umetuzidi
nguvu sana.”
17 Basi Isaki akatoka huko akajenga
kambi katika Bonde la Gerari, akaishi huko.
18 Ndipo Isaki akavichimbua tena vile visima
vya maji ambavyo vilichimbwa siku zile za
Abrahamu baba yake, ambavyo Wafilisti
walivifukia baada ya kufa Abrahamu,
akavipa majina yale yale ambayo baba yake
alikuwa amevipa.
19 Watumishi wa Isaki wakachimba
katika lile bonde wakagundua huko kisima
chenye maji safi. 20 Lakini wachungaji
wa Gerari wakagombana na wachungaji
wa Isaki wakisema, “Maji haya ni yetu!”
Ndipo akakiita kile kisima Eseki,[g] kwa
sababu waligombana naye. 21 Kisha
wakachimba kisima kingine, lakini hata
hicho pia wakakigombania, akakiita
Sitna.[h] 22 [i]Akaondoka huko, akachimba
kisima kingine, wala hakuna yeyote
aliyekigombania. Akakiita Rehobothi,[j]
akisema, “Sasa Bwana ametufanyia nafasi,
nasi tutastawi katika nchi.”
23 Kutoka pale akaenda Beer-Sheba.
24 [k]Usiku ule Bwana akamtokea,
akamwambia, “Mimi ndimi Mungu wa
Abrahamu baba yako. Usiogope, kwa maana
mimi niko pamoja nawe, nitakubariki na
kuongeza idadi ya wazao wako kwa ajili
ya Abrahamu mtumishi wangu.”
25 Isaki akajenga madhabahu huko,
akaliitia jina la Bwana. Akapiga hema lake
huko, nao watumishi wake wakachimba
kisima.
26 [l]Wakati huo, Abimeleki alikuwa
amemjia kutoka Gerari, akifuatana na
Ahuzathi mshauri wake, pamoja na
Fikoli jemadari wa majeshi yake. 27 Isaki
akawauliza, “Mbona mmekuja kwangu na
ninyi mlinichukia na kunifukuza?”
28 [m]Wakamjibu, “Tuliona wazi kuwa
Bwana alikuwa pamoja nawe, kwa
hiyo tukasema, ‘Inabidi kuwe na kiapo
cha mapatano kati yetu, kati yetu na
wewe. Na tufanye mkataba pamoja nawe
29 [n]kwamba hutatudhuru, kama jinsi nasi
hatukuwanyanyasa bali tuliwatendea
mema wakati wote na kuwaondoa kwetu
kwa amani. Tena sasa umebarikiwa na
Bwana.’ ”
30 [o]Basi Isaki akawaandalia karamu, nao
wakala na kunywa. 31 [p]Kesho yake asubuhi
na mapema, wakaapizana wao kwa wao.
Kisha Isaki akawaruhusu waende zao,
wakamwacha Isaki kwa amani.
32 [q]Siku hiyo watumishi wa Isaki
wakaja wakampa habari kuhusu

[a]**26:10** Mwa 12:8
[b]**26:11** 1Sam 24:6; 26:9; Za 105:15
[c]**26:12** Mt 13:8; Mwa 26:3
[d]**26:13** Mwa 13:2; Kum 8:18
[e]**26:14** Mwa 12:16; 24:36
[f]**26:15** Mwa 21:30; 21:25
[g]20 Eseki maana yake ni Ugomvi.
[h]21 Sitna maana yake Upinzani.
[i]**26:22** Kut 18:19; Mwa 17:6
[j]22 Rehobothi maana yake ni Mungu ametufanyia nafasi.
[k]**26:24** Mwa 24:12; 17:7
[l]**26:26** Mwa 21:22
[m]**26:28** Mwa 21:22
[n]**26:29** Mwa 31:29, 52; 24:31
[o]**26:30** Mwa 31:54; Kut 18:12
[p]**26:31** Mwa 21:23, 27
[q]**26:32** Mwa 21:30

kisima walichokuwa wamekichimba,
wakamwambia, “Tumepata maji!” 33 [a]Naye
akakiita Shiba,[b] mpaka leo mji huo unaitwa
Beer-Sheba.[c]
34 [d]Esau alipokuwa na umri wa miaka
arobaini, akamwoa Yudithi binti Beeri
Mhiti, kisha akamwoa Basemathi binti
Eloni Mhiti. 35 [e]Hawa walikuwa chanzo cha
huzuni ya Isaki na Rebeka.

*Yakobo Anaipata Baraka Ya Isaki*

27 Isaki alipokuwa mzee na macho yake
yalipokuwa yamekosa nguvu asiweze
kuona tena, akamwita Esau mwanawe
mkubwa, akamwambia, “Mwanangu.”
Akajibu, “Mimi hapa.”
2 Isaki akasema, “Mimi sasa ni mzee
na sijui siku ya kifo changu. 3 [f]Sasa basi,
chukua silaha zako, podo na upinde, uende
nyikani, ukawinde nyama pori kwa ajili
yangu. 4 Uniandalie aina ya chakula kitamu
nikipendacho uniletee nile, ili niweze
kukubariki kabla sijafa.”
5 Basi Rebeka alikuwa akisikiliza Isaki
alipokuwa akizungumza na mwanawe
Esau. Esau alipoondoka kwenda nyikani
kuwinda nyama pori na kuleta, 6 Rebeka
akamwambia Yakobo mwanawe, “Tazama,
nimemsikia baba yako akimwambia ndugu
yako Esau, 7 ‘Niletee mawindo, kisha
ukaniandalie chakula kitamu nile, ili niweze
kukubariki mbele za BWANA kabla sijafa.’
8 [g]Sasa, mwanangu, nisikilize kwa makini na
ufanye yale ninayokuambia: 9 Nenda sasa
katika kundi ukaniletee wana-mbuzi wawili
wazuri, ili niandalie chakula kitamu kwa
ajili ya baba yako, kama vile anavyopenda.
10 Kisha umpelekee baba yako ale, ili apate
kukubariki kabla hajafa.”
11 [h]Yakobo akamwambia Rebeka mama
yake, “Lakini ndugu yangu Esau ana
nywele mwilini, mimi nina ngozi nyororo.
12 [i]Itakuwaje kama baba yangu akinigusa?
Itaonekana kwake kama niliyemfanyia
ujanja na kuleta laana juu yangu badala
ya baraka.”
13 Mama yake akamwambia, “Mwanangu,
laana na iwe juu yangu. Fanya tu
ninalokuambia, nenda ukaniletee hao
wana-mbuzi.”
14 Kwa hiyo alikwenda akawaleta,
akampa mama yake, akaandaa chakula
kitamu, kama vile alivyopenda baba yake.
15 [j]Kisha Rebeka akachukua nguo nzuri za
Esau mwanawe wa kwanza, alizokuwa nazo
nyumbani, akamvika Yakobo mwanawe
mdogo. 16 Pia akamfunika mikononi na
sehemu laini ya shingo kwa ngozi za mbuzi.
17 Hatimaye akampa Yakobo hicho chakula
kitamu pamoja na mkate aliouoka.
18 Akamwendea baba yake akasema,
“Baba yangu.”
Akajibu, “Naam, mwanangu, wewe ni
nani?”
19 [k]Yakobo akamwambia baba yake,
“Mimi ni Esau mzaliwa wako wa kwanza.
Nimefanya kama ulivyoniambia. Tafadhali
uketi, ule sehemu ya mawindo yangu ili
uweze kunibariki.”
20 Isaki akamuuliza mwanawe.
“Umepataje haraka namna hii, mwanangu?”
Akajibu, “BWANA Mungu wako
amenifanikisha.”
21 [l]Kisha Isaki akamwambia Yakobo,
“Mwanangu tafadhali sogea karibu nami
ili nikupapase, nione kama hakika ndiwe
Esau mwanangu, au la.”
22 Yakobo akasogea karibu na baba yake
Isaki, ambaye alimpapasa na kusema, “Sauti
ni ya Yakobo, bali mikono ni ya Esau.”
23 [m]Hakumtambua, kwa sababu mikono yake
ilikuwa na nywele kama ya ndugu yake

[a]**26:33** Mwa 21:14
[b]33 Shiba kwa Kiebrania maana yake ni Saba.
[c]33 Beer-Sheba maana yake ni Kisima cha wale saba, yaani wale kondoo saba ambao Abrahamu aliwatoa kama ushahidi kati yake na Abimeleki.
[d]**26:34** Mwa 36:2
[e]**26:35** Mwa 27:46; Ay 7:16
[f]**27:3** Mwa 25:27
[g]**27:8** Mwa 27:13, 43
[h]**27:11** Mwa 25:25
[i]**27:12** Mwa 27:22
[j]**27:15** Mwa 27:27
[k]**27:19** Mwa 27:4
[l]**27:21** Mwa 27:12
[m]**27:23** Mwa 27:16

Esau, kwa hiyo akambariki. 24 Akamuuliza,
"Hivi kweli wewe ni mwanangu Esau?"
Akajibu, "Mimi ndiye."
25 [a]Kisha akasema, "Mwanangu, niletee
sehemu ya mawindo yako nile, ili nipate
kukubariki."
Yakobo akamletea naye akala, akamletea
na divai akanywa. 26 Kisha Isaki baba yake
akamwambia, "Njoo hapa, mwanangu,
unibusu."
27 [b]Kwa hiyo akamwendea akambusu.
Isaki aliposikia harufu ya nguo zake,
akambariki, akasema,

"Aha, harufu ya mwanangu
ni kama harufu ya shamba
ambalo BWANA amelibariki.
28 [c]Mungu na akupe umande kutoka
mbinguni
na utajiri wa duniani:
wingi wa nafaka na divai mpya.
29 [d]Mataifa na yakutumikie
na mataifa yakusujudie.
Uwe bwana juu ya ndugu zako,
na wana wa mama yako
wakusujudie.
Walaaniwe wale wakulaanio,
nao wale wakubarikio
wabarikiwe."

30 [e]Baada ya Isaki kumaliza kumbariki
na baada tu ya Yakobo kuondoka kwa
baba yake, ndugu yake Esau akaingia
kutoka mawindoni. 31 [f]Naye pia akaandaa
chakula kitamu akamletea baba yake. Kisha
akamwambia, "Baba yangu, keti ule sehemu
ya mawindo yangu, ili upate kunibariki."
32 [g]Isaki baba yake akamuuliza, "Wewe
ni nani?"
Akajibu, "Mimi ni mwanao, mzaliwa
wako wa kwanza, Esau."
33 [h]Isaki akatetemeka kwa nguvu sana,
akasema, "Alikuwa nani basi, ambaye
aliwinda mawindo akaniletea? Nilikula
kabla tu hujaja na nikambariki, naye hakika
atabarikiwa!"
34 [i]Esau aliposikia maneno haya ya baba
yake, akalia sauti kubwa na ya uchungu,
na kumwambia baba yake, "Nibariki mimi,
mimi pia, baba yangu!"
35 [j]Lakini akasema, "Ndugu yako amekuja
kwa udanganyifu na akachukua baraka
yako."
36 [k]Esau akasema, "Si ndiyo sababu
anaitwa Yakobo? Amenidanganya mara hizi
mbili: Alichukua haki yangu ya kuzaliwa
na sasa amechukua baraka yangu!" Kisha
akauliza, "Hukubakiza hata baraka moja
kwa ajili yangu?"
37 [l]Isaki akamjibu Esau, "Nimemfanya yeye
kuwa bwana juu yako, pia nimewafanya
ndugu zako wote kuwa watumishi wake,
nimemtegemeza kwa nafaka na divai
mpya. Sasa nitaweza kukufanyia nini,
mwanangu?"
38 [m]Esau akamwambia baba yake, "Je,
baba yangu una baraka moja tu? Unibariki
mimi pia, baba yangu!" Kisha Esau akalia
kwa sauti kubwa.
39 [n]Baba yake Isaki akamjibu,
akamwambia,

"Makao yako yatakuwa
mbali na utajiri wa dunia,
mbali na umande wa mbinguni
juu.
40 [o]Utaishi kwa upanga,
nawe utamtumikia ndugu yako,
lakini wakati utakapokuwa
umejikomboa,
utatupa nira yake
kutoka shingoni mwako."

*Yakobo Anakimbilia Kwa Labani*

41 [p]Esau akawa na kinyongo dhidi ya
Yakobo kwa ajili ya baraka ambazo baba

[a]**27:25** Mwa 27:4
[b]**27:27** Kut 4:27; Ebr 11:20
[c]**27:28** Kum 33:28; 33:11; 2Sam 1:21
[d]**27:29** Mwa 9:25; 25:23; 12:3
[e]**27:30** Mwa 31:54; Kut 18:12; 24:11
[f]**27:31** Mwa 21:23, 27
[g]**27:32** Mwa 27:18; 21:30
[h]**27:33** Mwa 21:14
[i]**27:34** Ebr 12:17; Kut 12:32
[j]**27:35** Yer 9:4
[k]**27:36** Mwa 25:26; Ebr 12:16-17
[l]**27:37** Mwa 27:28; Kum 16:13
[m]**27:38** Rut 1:9; Ebr 12:17
[n]**27:39** Ebr 11:20; Mwa 27:28
[o]**27:40** 2Sam 8:14; 2Fal 8:20-22
[p]**27:41** 1Sam 17:28; Hos 10:14

yake alikuwa amembariki. Akasema moyoni
mwake, “Siku za kuomboleza kwa ajili ya
baba yangu zimekaribia, ndipo nitamuua
ndugu yangu Yakobo.”
42 Rebeka alipokwisha kuambiwa yale
aliyoyasema Esau mwanawe mkubwa,
alimwita Yakobo mwanawe mdogo,
akamwambia, “Ndugu yako Esau
anajifariji kwa wazo la kukuua. 43 [a]Sasa
basi, mwanangu, fanya nisemalo: Kimbilia
haraka kwa Labani ndugu yangu kule
Harani. 44 Ukae naye kwa muda mpaka
ghadhabu ya ndugu yako itulie. 45 [b]Wakati
ndugu yako atakapokuwa hana hasira
nawe tena na amesahau uliyomtendea,
nitakupelekea ujumbe urudi. Kwa nini
niwapoteze wote wawili kwa siku moja?”
46 [c]Kisha Rebeka akamwambia Isaki,
“Nimechukia kuishi kwa sababu ya hawa
wanawake wa Kihiti. Ikiwa Yakobo ataoa
mke miongoni mwa wanawake wa nchi hii,
wanawake wa Kihiti kama hawa, sitakuwa
na faida kuendelea kuishi.”

28 [d]Basi Isaki akamwita Yakobo,
akambariki na akamwamuru, akisema,
“Usioe mwanamke wa Kikanaani. 2 Nenda
mara moja mpaka Padan-Aramu, kwenye
nyumba ya Bethueli baba wa mama yako.
Uchukue mke kati ya binti za Labani
ambaye ni ndugu wa mama yako. 3 [e]Mungu
Mwenyezi[f] na akubariki uwe na uzao
uongezeke idadi yako upate kuwa jamii
kubwa ya watu. 4 [g]Na akupe wewe na uzao
wako baraka aliyopewa Abrahamu, upate
kumiliki nchi unayoishi sasa kama mgeni,
nchi ambayo Mungu alimpa Abrahamu.”
5 [h]Kisha Isaki akamuaga Yakobo, naye
akaenda Padan-Aramu, kwa Labani mwana
wa Bethueli Mwaramu, ndugu wa Rebeka,
aliyekuwa mama wa Yakobo na Esau.

[a]**27:43** Mwa 24:29; 11:31
[b]**27:45** Mwa 26:3
[c]**27:46** Mwa 26:35; Ay 7:7
[d]**28:1** Mwa 24:3
[e]**28:3** Mwa 17:1; Hes 6:24
[f]3 Mungu Mwenyezi hapa ni jina la Kiebrania, El-Shaddai (yaani Mungu Mwenye utoshelevu wote).
[g]**28:4** Mwa 12:2, 3; 17:8
[h]**28:5** Hos 12:12; Mwa 24:29

6 Sasa Esau akajua kuwa Isaki amembariki
Yakobo na kumtuma kwenda Padan-
Aramu ili achukue mke huko na kwamba
alipombariki alimwamuru akisema, “Usioe
mke katika binti za Wakanaani,” 7 tena
kwamba Yakobo amewatii baba yake
na mama yake naye amekwenda Padan-
Aramu. 8 [i]Esau akatambua jinsi ambavyo
baba yake Isaki anavyowachukia binti za
Wakanaani. 9 Ndipo Esau akaenda kwa
Ishmaeli, akamwoa Mahalati, ndugu wa
Nebayothi na binti wa Ishmaeli mwana wa
Abrahamu, kuongezea wale wake wengine
aliokuwa nao.

*Ndoto Ya Yakobo Huko Betheli*

10 Yakobo akatoka Beer-Sheba kwenda
Harani. 11 Alipofika mahali fulani,
akalala hapo kwa sababu jua lilikuwa
limetua. Akachukua jiwe moja la mahali
pale, akaliweka chini ya kichwa chake
akajinyoosha akalala usingizi. 12 [j]Akaota
ndoto ambayo aliona ngazi imesimamishwa
juu ya ardhi, ncha yake ikiwa imefika
mbinguni na malaika wa Mungu wakawa
wakipanda na kushuka juu yake. 13 Juu
yake alisimama Bwana, akasema, “Mimi
ni Bwana, Mungu wa baba yako Abrahamu
na Mungu wa Isaki. Nchi ambayo umelala
juu yake, nitakupa wewe na uzao wako.
14 [k]Uzao wako utakuwa kama mavumbi ya
nchi, nawe utaenea upande wa magharibi
na mashariki, kaskazini na kusini. Kupitia
wewe na uzao wako mataifa yote ya
duniani yatabarikiwa. 15 [l]Niko pamoja
nawe nami nitakulinda kila uendako na
nitakurudisha katika nchi hii. Sitakuacha
mpaka nitakapofanya hayo niliyokuahidi.”
16 [m]Yakobo alipoamka kutoka usingizini,
akawaza, “Hakika Bwana yuko mahali
hapa, wala mimi sikujua.” 17 [n]Kwa hiyo
akaogopa, akasema, “Mahali hapa panatisha
kama nini! Bila shaka hapa ndipo nyumba
ya Mungu ilipo, hili ni lango la mbinguni.”

[i]**28:8** Mwa 26:35
[j]**28:12** Yn 1:51
[k]**28:14** Mwa 26:4; 12:3; Gal 3:8
[l]**28:15** Kum 31:6, 8; Law 26:42; Za 105:10
[m]**28:16** 1Fal 3:15; Yer 31:26
[n]**28:17** Kut 3:5; Yos 5:15

18 Asubuhi yake na mapema, Yakobo
akalichukua lile jiwe aliloliweka chini ya
kichwa chake, akalisimamisha kama nguzo
na kumimina mafuta juu yake. 19 [a]Mahali
pale akapaita Betheli,[b] ingawa mji ule hapo
kwanza uliitwa Luzu.
20 [c]Kisha Yakobo akaweka nadhiri,
akisema, "Kama Mungu akiwa pamoja
nami na kunilinda katika safari niendayo,
akinipa chakula nile na nguo nivae 21 [d]na
nirudi salama nyumbani kwa baba yangu,
hapo ndipo BWANA atakuwa Mungu wangu,
22 [e]nalo jiwe hili nililolisimamisha kama
nguzo litakuwa nyumba ya Mungu na
katika yote utakayonipa nitakutolea wewe
sehemu ya kumi."

### *Yakobo Awasili Padan-Aramu*

29 [f]Kisha Yakobo akaendelea na safari
yake na akafika kwenye nchi za
mataifa ya mashariki. 2 Huko akaona kisima
katika shamba, pamoja na makundi matatu
ya kondoo yamelala karibu na kisima
hicho kwa sababu walikuwa wanakunywa
maji kutoka kwenye kisimani hicho. Jiwe
lililokuwa mdomoni mwa kisima lilikuwa
kubwa. 3 Wakati kondoo wanapokuwa
wamekusanyika hapo, wachungaji
huvingirisha jiwe hilo kutoka kwenye
mdomo wa kisima na kunywesha kondoo.
Kisha hulirudisha jiwe mahali pake juu ya
mdomo wa kisima.
4 [g]Yakobo aliwauliza wachungaji, "Ndugu
zangu, ninyi mmetoka wapi?"
Wakamjibu, "Tumetoka Harani."
5 Aliwaambia, "Je, mnamjua Labani,
mjukuu wa Nahori?"
Wakamjibu, "Ndiyo, tunamfahamu."
6 [h]Kisha Yakobo akawauliza, "Je, yeye
ni mzima?"
Wakasema, "Ndiyo, ni mzima, na hapa
yuaja Raheli binti yake akiwa na kondoo."
7 Akasema, "Tazama, jua bado liko juu, si
wakati wa kukusanya mifugo. Nywesheni
kondoo na mwarudishe malishoni."
8 Walijibu, "Haiwezekani, mpaka
kondoo wote wakusanyike na jiwe liwe
limevingirishwa kutoka mdomo wa kisima.
Ndipo tutanywesha kondoo."
9 Alipokuwa akizungumza nao, Raheli
akaja pamoja na kondoo wa baba yake, kwa
maana alikuwa mchunga kondoo. 10 Yakobo
alipomwona Raheli binti Labani, ndugu wa
mama yake, pamoja na kondoo wa Labani,
alikwenda na kulivingirisha jiwe kutoka
mdomoni mwa kisima na kuwanywesha
kondoo wa mjomba wake. 11 [i]Kisha Yakobo
akambusu Raheli na akaanza kulia kwa
sauti. 12 [j]Yakobo alikuwa amemwambia
Raheli kuwa yeye alikuwa jamaa ya baba
yake, na kwamba ni mwana wa Rebeka.
Basi Raheli alikimbia na kumweleza baba
yake.
13 [k]Mara Labani aliposikia habari
kuhusu Yakobo, mwana wa ndugu
yake, aliharakisha kwenda kumlaki.
Akamkumbatia na kumbusu, halafu
akamleta nyumbani kwake, kisha Yakobo
akamwambia mambo yote. 14 [l]Ndipo Labani
akamwambia, "Wewe ni nyama yangu na
damu yangu mwenyewe."

### *Yakobo Awaoa Lea Na Raheli*

Baada ya Yakobo kukaa kwa Labani
mwezi mzima, 15 Labani akamwambia,
"Kwa vile wewe ni jamaa yangu, ndiyo
sababu unifanyie kazi bila ujira? Niambie
ujira wako utakuwa nini."
16 [m]Labani alikuwa na binti wawili,
binti mkubwa aliitwa Lea na binti mdogo
aliitwa Raheli. 17 Lea alikuwa na macho
dhaifu, lakini Raheli alikuwa na umbo la
kupendeza na mzuri wa sura. 18 [n]Yakobo
akampenda Raheli, akamwambia Labani,
"Nitakutumikia kwa miaka saba kwa ajili
ya kumpata Raheli binti yako mdogo."

---

[a] **28:19** Yos 16:2; Amu 1:23, 26
[b] 19 Betheli maana yake Nyumba ya Mungu.
[c] **28:20** Mwa 31:13; Amu 1:23, 26
[d] **28:21** Kum 26:17; Za 48:14; 118:28
[e] **28:22** Mwa 14:20; Lk 18:12
[f] **29:1** Mwa 25:6
[g] **29:4** Mwa 42:7; Amu 19:17
[h] **29:6** Mwa 30:22-27; Kut 2:16
[i] **29:11** Mwa 33:4
[j] **29:12** Mwa 24:28; Lk 15:20
[k] **29:13** Mwa 24:29; Lk 15:20
[l] **29:14** Amu 9:2; Isa 58:7
[m] **29:16** Mwa 30:9; Rut 4:2, 11
[n] **29:18** Mwa 24:67; Hos 12:12

19 Labani akasema, “Ni bora zaidi nikupe
Raheli kuliko kumpa mtu mwingine yeyote.
Kaa pamoja na mimi hapa.” 20 Kwa hiyo
Yakobo akatumika miaka saba ili kumpata
Raheli, lakini ilionekana kwake kama siku
chache tu kwa sababu ya upendo wake kwa
Raheli.

21 [a]Ndipo Yakobo akamwambia
Labani, “Nipe mke wangu. Muda wangu
umekamilika, nami nataka nikutane naye
kimwili.”

22 [b]Basi Labani akaalika watu wote wa
mahali pale na akafanya karamu.

23 Lakini ilipofika jioni, akamchukua Lea
binti yake akampa Yakobo, naye Yakobo
akakutana naye kimwili. 24 Naye Labani
akamtoa Zilpa, mtumishi wake wa kike,
kuwa mtumishi wa Lea, binti yake.

25 [c]Kesho yake asubuhi, Yakobo
akagundua kuwa amepewa Lea! Basi Yakobo
akamwambia Labani, “Ni jambo gani hili
ulilonitendea? Nilikutumikia kwa ajili ya
Raheli, sivyo? Kwa nini umenidanganya?”

26 [d]Labani akajibu, “Si desturi yetu
kumwoza binti mdogo kabla ya kumwoza
binti mkubwa. 27 Maliza juma la arusi ya
binti huyu, kisha pia nitakupa huyu binti
mdogo, kwa kutumika miaka mingine
saba.”

28 Naye Yakobo akafanya hivyo.
Akamaliza juma na Lea, kisha Labani
akampa Raheli binti yake kuwa mke wake.
29 [e]Labani akamtoa Bilha mtumishi wake wa
kike kwa Raheli ili kuwa mtumishi wake.
30 Pia Yakobo akakutana na Raheli kimwili,
naye akampenda Raheli zaidi kuliko Lea.
Yakobo akamtumikia Labani kwa miaka
mingine saba.

### *Wana Wa Yakobo*

31 [f]BWANA alipoona kwamba Lea
hapendwi, akampa watoto, lakini Raheli
alikuwa tasa. 32 [g]Lea akapata mimba akazaa
mwana. Akamwita Reubeni,[h] kwa maana
alisema, “Ni kwa sababu BWANA ameona
huzuni yangu. Hakika mume wangu sasa
atanipenda.”

33 [i]Akapata tena mimba, naye alipozaa
mwana, akasema, “Kwa sababu BWANA
alisikia kwamba sipendwi, amenipa
tena huyu mwana.” Kwa hiyo akamwita
Simeoni.[j]

34 Akapata tena mimba, naye alipozaa
mwana, akasema, “Sasa afadhali mume
wangu ataambatana na mimi, kwa sababu
nimemzalia wana watatu.” Kwa hiyo
akamwita Lawi.[k]

35 [l]Akapata tena mimba, naye alipozaa
mwana, akasema, “Wakati huu nitamsifu
BWANA.” Kwa hiyo akamwita Yuda.[m] Kisha
akaacha kuzaa watoto.

30 Raheli alipoona hamzalii Yakobo
watoto, akamwonea ndugu yake wivu.
Hivyo akamwambia Yakobo, “Nipe watoto,
la sivyo nitakufa!”

2 [n]Yakobo akamkasirikia, akamwambia,
“Je, mimi ni badala ya Mungu, ambaye
amekuzuia usizae watoto?”

3 [o]Ndipo Raheli akamwambia, “Hapa
yupo Bilha, mtumishi wangu wa kike.
Kutana naye kimwili ili aweze kunizalia
watoto na kwa kupitia yeye mimi pia
niweze kuwa na uzao.”

4 [p]Hivyo Raheli akampa Yakobo Bilha awe
mke wake. Yakobo akakutana naye kimwili,
5 Bilha akapata mimba, naye akamzalia
Yakobo mwana. 6 [q]Ndipo Raheli akasema,
“Mungu amenipa haki yangu, amesikiliza

---

[a]**29:21** Amu 15:1
[b]**29:22** Amu 14:10; Yn 2:1-2
[c]**29:25** Mwa 12:18; 27:36
[d]**29:26** 1Sam 14:49; 2Sam 6:23
[e]**29:29** 1Nya 5:1; Mwa 16:1
[f]**29:31** Kum 21:15-17; Za 127:3
[g]**29:32** Mwa 30:23; Hes 1:5
[h]32 Reubeni maana yake Ona mwana, yaani Yehova ameangalia taabu yangu.
[i]**29:33** Kut 6:15; 1Nya 4:24
[j]33 Simeoni maana yake Anasikia, yaani sasa ataungana nami kama Raheli.
[k]34 Lawi maana yake Nimeunganishwa, yaani na mume wangu.
[l]**29:35** Mwa 49:8; Mt 1:2-3
[m]35 Yuda maana yake Sifa, yaani Nitamsifu Yehova.
[n]**30:2** 2Fal 5:7; Mwa 16:2
[o]**30:3** Mwa 16:2
[p]**30:4** Mwa 16:3-4
[q]**30:6** Za 35:24; 1Sam 1:20; Yos 19:40

maombi yangu na kunipa mwana." Kwa
sababu hiyo akamwita Dani.[a]
7 Bilha mtumishi wa kike wa Raheli
akapata mimba tena, akamzalia Yakobo
mwana wa pili. 8 [b]Ndipo Raheli akasema,
"Nilikuwa na mashindano makubwa na
ndugu yangu, nami nimeshinda." Kwa hiyo
akamwita Naftali.[c]
9 [d]Lea alipoona kuwa amekoma kuzaa
watoto, alimchukua mtumishi wake wa kike
Zilpa, naye akampa Yakobo awe mke wake.
10 Mtumishi wa Lea yaani Zilpa, akamzalia
Yakobo mwana. 11 [e]Ndipo Lea akasema, "Hii
ni bahati nzuri aje!" Kwa hiyo akamwita
Gadi.
12 Mtumishi wa kike wa Lea akamzalia
Yakobo mwana wa pili. 13 [f]Ndipo Lea
aliposema, "Jinsi gani nilivyo na furaha!
Wanawake wataniita furaha." Kwa hiyo
akamwita Asheri.[g]
14 [h]Wakati wa kuvuna ngano, Reubeni
akaenda shambani akakuta tunguja, ambazo
alizileta kwa Lea mama yake. Raheli
akamwambia Lea, "Tafadhali nakuomba
unipe baadhi ya tunguja za mwanao."
15 [i]Lakini Lea akamwambia,
"Haikukutosha kumtwaa mume wangu? Je,
utachukua na tunguja za mwanangu pia?"
Raheli akasema, "Vema sana! Yakobo
atakutana nawe kimwili leo usiku, kwa
malipo ya tunguja za mwanao."
16 Kwa hiyo Yakobo alipokuja kutoka
shambani jioni ile, Lea akaenda kumlaki,
akamwambia, "Lazima ukutane nami
kimwili. Nimekukodisha kwa tunguja za
mwanangu." Kwa hiyo akakutana naye
kimwili usiku ule.
17 [j]Mungu akamsikiliza Lea, naye akapata
mimba akamzalia Yakobo mwana wa
tano. 18 [k]Ndipo Lea akasema, "Mungu
amenizawadia kwa kumpa mume wangu
mtumishi wangu wa kike." Kwa hiyo
akamwita Isakari.[l]
19 Lea akapata mimba tena akamzalia
Yakobo mwana wa sita. 20 [m]Ndipo Lea
aliposema, "Mungu amenizawadia kwa
zawadi ya thamani sana. Wakati huu
mume wangu ataniheshimu kwa sababu
nimemzalia wana sita." Kwa hiyo akamwita
Zabuloni.[n]
21 [o]Baadaye akamzaa mtoto wa kike
akamwita Dina.[p]
22 [q]Ndipo Mungu akamkumbuka Raheli,
akasikia maombi yake na akafungua tumbo
lake. 23 [r]Akapata mimba na akamzaa mwana
na kusema, "Mungu ameniondolea aibu
yangu."
24 [s]Akamwita Yosefu[t] na kusema, "BWANA
na anipe mwana mwingine."

*Makundi Ya Yakobo Yaongezeka*

25 [u]Baada ya Raheli kumzaa Yosefu,
Yakobo akamwambia Labani, "Nipe
ruhusa nirudi katika nchi yangu. 26 Nipe
wake zangu na watoto, ambao nimetumika
kuwapata, nami niende zangu. Unajua ni
kazi kiasi gani ambayo nimekufanyia."
27 [v]Lakini Labani akamwambia, "Ikiwa
nimepata kibali machoni pako, tafadhali
ukae. Nimegundua kwa njia ya uaguzi
kwamba BWANA amenibariki kwa sababu
yako." 28 [w]Akaongeza kumwambia, "Taja
ujira wako nami nitakulipa."

---

[a]6 Dani maana yake Anahukumu, yaani Mungu amenipa haki yangu.
[b]**30:8** Hos 12:3-4; Hes 1:42
[c]8 Naftali maana yake Nimeshindana nami nimeshinda.
[d]**30:9** Mwa 29:16
[e]**30:11** Mwa 35:26; Kut 1:4
[f]**30:13** Lk 1:48
[g]13 Asheri maana yake Nimefurahi, yaani Mungu amenifurahisha.
[h]**30:14** Wim 7:13
[i]**30:15** Isa 7:13
[j]**30:17** Mwa 25:21
[k]**30:18** Hes 1:8, 24
[l]18 Isakari maana yake Zawadi, yaani Mungu amenizawadia.
[m]**30:20** 1Pet 3:7
[n]20 Zabuloni maana yake Heshima.
[o]**30:21** Mwa 34:1
[p]21 Dina maana yake Tetea haki, yaani Mungu amenitetea katika mashindano yangu.
[q]**30:22** Mwa 11:30
[r]**30:23** Isa 4:1; Lk 1:25
[s]**30:24** Mwa 35:17
[t]24 Yosefu maana yake Yeye na aongeze, yaani Mungu na aniongezee.
[u]**30:25** Mwa 24:54
[v]**30:27** Mwa 26:24
[w]**30:28** Mwa 29:15

[29] Yakobo akamwambia, “Unajua jinsi
ambavyo nimekutumikia na jinsi ambavyo
wanyama wako walivyolishwa vizuri chini
ya uangalizi wangu. [30] Kidogo ulichokuwa
nacho kabla sijaja kimeongezeka sana, naye
BWANA amekubariki popote nilipokuwa.
Lakini sasa, ni lini nitashughulikia mambo
ya nyumba yangu mwenyewe?”
[31] Labani akamuuliza, “Nikupe nini?”
Yakobo akamjibu, “Usinipe chochote
lakini kama utanifanyia jambo hili moja,
nitaendelea kuchunga na kuyaangalia
makundi yako. [32] [a]Niruhusu nipite katika
makundi yako yote leo niondoe humo kila
kondoo mwenye mabakabaka au madoadoa,
kila mwana-kondoo mweusi na kila mbuzi
mwenye madoadoa au mabakabaka.
Hawa watakuwa ujira wangu. [33] Uadilifu
wangu utanishuhudia siku zijazo, kila
utakapochunguza ujira ambao umenilipa
mimi. Mbuzi yeyote wangu ambaye hana
mabakabaka wala madoadoa, au mwana-kondoo ambaye si mweusi, atahesabika
ameibwa.”
[34] Labani akasema, “Ninakubali na iwe
kama ulivyosema.” [35] Siku ile ile Yakobo
akawaondoa beberu wote waliokuwa na
mistari au madoadoa na mbuzi wake wote
waliokuwa na mistari au madoadoa (wote
waliokuwa na alama nyeupe juu yao) na
wana-kondoo weusi wote, akawaweka chini
ya uangalizi wa wanawe. [36] Kisha Labani
akamwacha Yakobo kwa mwendo wa safari
ya siku tatu kati yake na Yakobo, wakati
Yakobo akiendelea kuchunga lile kundi la
Labani lililobaki.
[37] [b]Hata hivyo, Yakobo, akachukua fito
mbichi zilizokatwa wakati huo huo za
miti ya mlubna, mlozi na mwaramoni
akazibambua ili mistari myeupe ionekane
katika fito hizo. [38] [c]Kisha akaweka fito
alizozibambua kwenye mabirika yote
ya kunyweshea mifugo, ili ziwe mbele
ya makundi walipokuja kunywa maji.
Wanyama walipokuja kunywa maji, hali
wakiwa wanahitaji mbegu, [39] wakapandwa
hizo fito zikiwa mbele yao. Wanyama
waliopata mimba mbele ya hizo fito walizaa
wanyama wenye mistari, madoadoa na
mabakabaka. [40] Yakobo akawatenga wadogo
wa kundi peke yao, lakini akazielekeza
nyuso za hao waliobaki kwenye wale
wenye mistari na weusi waliokuwa mali
ya Labani. Hivyo akatenga makundi yake
mwenyewe, na wala hakuwachanganya na
wanyama wa Labani. [41] Kila mara wanyama
wenye nguvu walipohitaji mbegu, Yakobo
aliweka zile fito kwenye mabirika mbele
ya hao wanyama, ili wapandwe karibu na
hizo fito, [42] lakini ikiwa wanyama walikuwa
wadhaifu hakuziweka hizo fito. Hivyo
wanyama wadhaifu wakawa wa Labani,
na wanyama wenye nguvu wakawa wa
Yakobo. [43] [d]Kwa njia hii Yakobo akastawi
sana, tena akawa na makundi makubwa,
watumishi wa kike na wa kiume na ngamia
na punda.

*Yakobo Akimbia Kutoka Kwa Labani*

31 Yakobo akawasikia wana wa Labani
wakisema, “Yakobo amechukua kila
kitu kilichokuwa cha baba yetu naye
amepata utajiri huu wote kutokana na vile
vilivyokuwa mali ya baba yetu.” [2] Yakobo
akatambua kwamba moyo wa Labani kwake
haukuwa kama ulivyokuwa mwanzo.
[3] [e]Ndipo BWANA akamwambia Yakobo,
“Rudi katika nchi ya baba zako na kwa
watu wako, nami nitakuwa pamoja nawe.”
[4] Hivyo Yakobo akatuma ujumbe kwa
Raheli na Lea waje machungani yalikokuwa
makundi yake. [5] [f]Akawaambia, “Naona
moyo wa baba yenu kwangu sivyo kama
ulivyokuwa mwanzoni, lakini Mungu
wa baba yangu amekuwa pamoja nami.
[6] [g]Mnajua kwamba nimemtumikia baba
yenu kwa nguvu zangu zote, [7] [h]hata hivyo
baba yenu amenidanganya kwa kubadilisha
ujira wangu mara kumi. Hata hivyo, Mungu
hakumruhusu kunidhuru. [8] [i]Kama alisema,
‘Wenye madoadoa watakuwa ujira wako,’

[a]**30:32** Mwa 31:8, 12
[b]**30:37** Yer 1:11
[c]**30:38** Kut 2:16
[d]**30:43** Mwa 12:16
[e]**31:3** Mwa 32:9; 21:22
[f]**31:5** Mwa 21:22; 26:3
[g]**31:6** Mwa 30:29
[h]**31:7** Mwa 31:41
[i]**31:8** Mwa 30:32

basi makundi yote yalizaa wenye madoadoa,
kama alisema, ‘Wenye mistari watakuwa
ujira wako,’ basi makundi yote yalizaa
wenye mistari. 9 Hivyo Mungu amechukua
mifugo ya baba yenu na amenipa mimi.
10 “Wakati fulani majira ya kuzaliana
niliota ndoto ambayo niliinua macho na
kuona kwamba wale mabeberu waliokuwa
wakipanda kundi walikuwa wa mistari,
madoadoa na mabakabaka. 11 Malaika wa
Mungu akaniambia katika ndoto, ‘Yakobo.’
Nikamjibu, ‘Mimi hapa.’ 12 [a]Akasema,
‘Inua macho yako uone wale mabeberu
wote wanaopanda kundi wana mistari,
madoadoa au mabakabaka, kwa maana
nimeona yale yote ambayo Labani amekuwa
akikutendea. 13 [b]Mimi ndiye Mungu wa
Betheli, ulikomiminia ile nguzo mafuta na
pale mahali uliponiwekea nadhiri. Sasa
ondoka katika nchi hii mara moja urudi
katika nchi uliyozaliwa.’ ”
14 Ndipo Raheli na Lea wakajibu, “Je
bado tu tunalo fungu lolote katika urithi
wa nyumba ya baba yetu? 15 [c]Je, yeye
hatuhesabu sisi kama wageni? Sio kwamba
ametuuza tu, bali ametumia hata na vile
vilivyolipwa kwa ajili yetu. 16 Hakika
utajiri wote ambao Mungu ameuchukua
kutoka kwa baba yetu ni mali yetu na
watoto wetu. Hivyo fanya lolote lile Mungu
alilokuambia.”
17 Ndipo Yakobo akawapandisha watoto
wake na wake zake juu ya ngamia, 18 [d]naye
akawaswaga wanyama wote mbele yake
pamoja na vitu vyote alivyokuwa amechuma
huko Padan-Aramu kwenda kwa baba yake
Isaki katika nchi ya Kanaani.
19 [e]Labani alipokuwa amekwenda kukata
kondoo wake manyoya, Raheli aliiba
miungu ya nyumba ya baba yake. 20 [f]Zaidi
ya hayo, Yakobo alimdanganya Labani
Mwaramu kwa kutokumwambia kwamba
anakimbia. 21 [g]Hivyo akakimbia pamoja na
vitu vyote alivyokuwa navyo na kuvuka
Mto Frati akaelekea nchi ya vilima katika
Gileadi.

*Labani Amfuatilia Yakobo*

22 [h]Siku ya tatu Labani akaambiwa kwamba
Yakobo amekimbia. 23 [i]Akiwachukua
jamaa zake, akamfuatia Yakobo kwa siku
saba na kumkuta kwenye nchi ya vilima
katika Gileadi. 24 [j]Ndipo Mungu akamjia
Labani Mwaramu katika ndoto usiku na
kumwambia, “Jihadhari usiseme neno
lolote kwa Yakobo, liwe zuri au baya.”
25 [k]Yakobo alikuwa amepiga hema lake
katika nchi ya vilima katika Gileadi wakati
Labani alipomkuta, Labani na jamaa yake
wakapiga kambi huko pia. 26 [l]Ndipo Labani
akamwambia Yakobo, “Umefanya nini?
Umenidanganya na umewachukua binti
zangu kama mateka katika vita. 27 [m]Kwa
nini ulikimbia kwa siri na kunidanganya?
Kwa nini hukuniambia ili nikuage kwa
furaha na nyimbo za matari na vinubi?
28 [n]Hata hukuniruhusu niwabusu wajukuu
zangu na kuwaaga binti zangu. Umefanya
kitu cha kipumbavu. 29 Nina uwezo wa
kukudhuru, lakini usiku uliopita Mungu
wa baba yako alisema nami, akaniambia,
‘Jihadhari, usiseme neno lolote kwa Yakobo
liwe zuri au baya.’ 30 [o]Sasa umeondoka kwa
sababu umetamani kurudi nyumbani kwa
baba yako. Lakini kwa nini umeiba miungu
yangu?”
31 Yakobo akamjibu Labani, “Niliogopa,
kwa sababu nilifikiri ungeweza
kuninyang’anya binti zako kwa nguvu.
32 [p]Lakini kama ukimkuta yeyote aliye na
miungu yako, hataishi. Mbele ya jamaa
yetu, angalia mwenyewe uone kama kuna
chochote chako hapa nilicho nacho, kama
kipo, kichukue.” Basi Yakobo hakujua

[a]**31:12** Kut 3:7
[b]**31:13** Mwa 28:10-22
[c]**31:15** Mwa 29:20
[d]**31:18** Mwa 35:27
[e]**31:19** Amu 17:5; Hos 3:4
[f]**31:20** Mwa 27:36
[g]**31:21** Kut 2:15
[h]**31:22** Mwa 30:36
[i]**31:23** Kut 14:9
[j]**31:24** Mwa 20:3; 24:50
[k]**31:25** Mwa 31:21
[l]**31:26** 1Sam 30:23
[m]**31:27** Mwa 31:20
[n]**31:28** Mwa 27:27
[o]**31:30** Mwa 31:19
[p]**31:32** Mwa 44:9

kwamba Raheli alikuwa ameiba hiyo
miungu.
33 Kwa hiyo Labani akaingia ndani ya
hema la Yakobo na ndani ya hema la Lea
na ndani ya hema la watumishi wawili wa
kike, lakini hakukuta chochote. Baadaye
alipotoka katika hema la Lea, akaingia
hema la Raheli. 34 Basi Raheli ndiye alikuwa
amechukua ile miungu ya nyumbani kwao
na kuiweka katika matandiko ya ngamia
na kukalia. Labani akatafuta kila mahali
kwenye hema lakini hakupata chochote.
35 [a]Raheli akamwambia baba yake,
"Usikasirike, bwana wangu kwa kuwa
siwezi kusimama ukiwepo, niko katika
hedhi." Labani akatafuta lakini hakuweza
kuipata miungu ya nyumbani kwake.
36 Yakobo akakasirika na kumshutumu
Labani, akisema, "Uhalifu wangu ni nini?"
Akamuuliza Labani, "Ni dhambi gani
niliyofanya hata unaniwinda? 37 [b]Sasa kwa
kuwa umepekua vitu vyangu vyote umepata
nini kilicho cha nyumbani mwako? Kiweke
hapa mbele ya jamaa yako na yangu, nao
waamue kati yetu sisi wawili.
38 "Mpaka sasa nimekuwa pamoja nawe
miaka ishirini. Kondoo wako na mbuzi wako
hawajaharibu mimba, wala sijala kondoo
dume kutoka makundi yako. 39 [c]Sikukuletea
mfugo aliyeraruliwa na wanyama pori,
nilibeba hasara mimi mwenyewe. Tena
ulinidai malipo kwa chochote kilichoibwa
mchana au usiku. 40 Hii ndiyo iliyokuwa
hali yangu: Niliumia kwa joto la mchana na
baridi usiku, pia usingizi ulinipa. 41 [d]Ilikuwa
hivi kwa miaka ile ishirini niliyokuwa
nyumbani kwako. Nilikutumikia miaka
ile kumi na minne kwa ajili ya binti zako
wawili, miaka sita kwa ajili ya makundi
yako, nawe ulibadilisha ujira wangu mara
kumi. 42 [e]Kama Mungu wa baba yangu,
Mungu wa Abrahamu na Hofu ya Isaki,
hakuwa pamoja nami, hakika ungenifukuza
mikono mitupu. Lakini Mungu ameona
taabu yangu na kazi ngumu ya mikono
yangu, naye usiku uliopita amekukemea."
43 Labani akamjibu Yakobo, "Wanawake
hawa ni binti zangu, watoto hawa ni watoto
wangu na makundi haya ni makundi yangu.
Vyote unavyoviona ni vyangu. Lakini hata
hivyo ninaweza kufanya nini kuhusu hawa
binti zangu, au kuhusu watoto waliowazaa?
44 [f]Njoo sasa na tufanye agano, wewe na
mimi, na liwe kama shahidi kati yetu."
45 [g]Hivyo Yakobo akachukua jiwe,
akalisimamisha kama nguzo. 46 [h]Akawaambia
jamaa yake, "Kusanyeni mawe." Hivyo
wakachukua mawe na kuyakusanya yakawa
lundo, wakala chakula hapo karibu na hilo
lundo. 47 [i]Labani akaliita Yegar-Sahadutha[j]
na Yakobo akaliita Galeedi.[k]
48 [l]Labani akasema, "Lundo hili ni shahidi
kati yako na mimi leo." Ndiyo maana
likaitwa Galeedi. 49 [m]Pia liliitwa Mispa,[n] kwa
sababu alisema, "BWANA na aweke ulinzi
kati yako na mimi wakati kila mmoja akiwa
mbali na mwingine. 50 [o]Kama ukiwatenda
mabaya binti zangu au ukioa wake wengine
zaidi ya binti zangu, hata ingawa hakuna
hata mmoja aliye pamoja nasi, kumbuka
kwamba Mungu ni shahidi kati yako na
mimi."
51 [p]Pia Labani akamwambia Yakobo,
"Hili ndilo lundo, na hii ndiyo nguzo
niliyoisimamisha kati yako na mimi.
52 [q]Lundo hili ni shahidi na nguzo hii ni
shahidi, kwamba sitavuka lundo hili kuja
upande wako kukudhuru, nawe kwamba
hutavuka lundo hili na nguzo hii kuja
upande wangu kunidhuru. 53 [r]Mungu wa

[a]**31:35** Law 19:3, 32
[b]**31:37** Mwa 31:23
[c]**31:39** Kut 22:13
[d]**31:41** Mwa 29:30; 31:7
[e]**31:42** Mwa 31:53

[f]**31:44** Mwa 21:27
[g]**31:45** Mwa 28:18
[h]**31:46** Mwa 31:48, 52
[i]**31:47** Mwa 21:30
[j]47 Yegar-Sahadutha maana yake ni Lundo la ushahidi kwa Kiaramu.
[k]47 Galeedi maana yake ni Lundo la ushahidi kwa Kiebrania.
[l]**31:48** Mwa 31:46
[m]**31:49** Amu 11:29
[n]49 Mispa maana yake Mnara wa ulinzi.
[o]**31:50** Yer 29:23; 42:5
[p]**31:51** Mwa 28:18
[q]**31:52** Mwa 21:30
[r]**31:53** Mwa 16:5; 31:42

Abrahamu na Mungu wa Nahori, Mungu
wa baba zao, aamue kati yetu."

Hivyo Yakobo akaapa kwa jina la Hofu ya
baba yake Isaki. 54 Yakobo akatoa dhabihu
juu ya kilima na akawaalika jamaa zake
kula chakula. Baada ya kula, wakalala
huko.

55 Kesho yake asubuhi na mapema,
Labani akawabusu wajukuu zake, binti zake
na kuwabariki. Kisha akaondoka, akarudi
nyumbani.

*Yakobo Ajiandaa Kukutana Na Esau*

32 Yakobo pia akaondoka akaenda zake,
nao malaika wa Mungu wakakutana
naye. 2 Yakobo alipowaona, akasema, "Hii
ni kambi ya Mungu!" Kwa hiyo akapaita
mahali pale Mahanaimu.[a]

3 [b]Yakobo akatuma wajumbe kumtangulia
kwa Esau ndugu yake huko Seiri, katika
nchi ya Edomu. 4 [c]Akawaagiza akisema:
"Hili ndilo mtakalomwambia bwana wangu
Esau: 'Mtumishi wako Yakobo anasema,
nimekuwa nikiishi pamoja na Labani na
nimekuwako huko mpaka sasa. 5 [d]Ninao
ng'ombe na punda, kondoo na mbuzi,
watumishi wa kiume na wa kike. Sasa
ninatuma ujumbe huu kwa bwana wangu,
ili nipate kibali machoni pako.' "

6 [e]Wajumbe waliporudi kwa Yakobo,
wakamwambia, "Tulikwenda kuonana
na ndugu yako Esau, naye sasa anakuja
kukulaki akifuatana na wanaume 400."

7 Kwa hofu kuu na huzuni, Yakobo
akagawanya watu aliokuwa nao katika
makundi mawili, pia akagawanya makundi
ya kondoo na mbuzi, na vilevile ng'ombe
na ngamia. 8 Yakobo alifikiri, "Kama Esau
akija na kushambulia kundi moja, kundi
lililobaki litaweza likanusurika."

9 [f]Ndipo Yakobo akaomba, "Ee Mungu
wa baba yangu Abrahamu, Mungu wa baba
yangu Isaki, Ee BWANA, ambaye uliniambia,
'Rudi katika nchi yako na jamaa yako,
nami nitakufanya ustawi,' 10 [g]mimi sistahili
fadhili na uaminifu wako wote ulionitendea
mimi mtumishi wako. Nilikuwa na fimbo tu
mkononi mwangu nilipovuka mto huu wa
Yordani, lakini sasa ninayo makundi mawili.
11 [h]Nakuomba, uniokoe na mkono wa ndugu
yangu Esau, kwa maana ninaogopa kuwa
atakuja kunishambulia, pia mama pamoja
na watoto wao. 12 [i]Lakini umeshasema,
'Hakika nitakufanya ustawi na kuufanya
uzao wako kuwa mwingi kama mchanga
wa baharini ambao hauwezi kuhesabika!' "

13 [j]Akalala pale usiku ule, miongoni
mwa vitu alivyokuwa navyo, akachagua
zawadi kwa ajili ya Esau ndugu yake:
14 [k]Mbuzi waume ishirini na mbuzi wake
200, kondoo dume ishirini na kondoo wake
200. 15 [l]Ngamia wake thelathini pamoja
na ndama zao, ng'ombe wake arobaini
na mafahali kumi, punda wake ishirini na
punda waume kumi. 16 [m]Akaviweka chini ya
uangalizi wa watumishi wake, kila kundi
peke yake na kuwaambia, "Nitanguliéni na
kuacha nafasi kati ya makundi."

17 Akamwagiza yule aliyetangulia kuwa,
"Ndugu yangu Esau atakapokutana nawe na
kukuuliza, 'Wewe ni wa nani? Unakwenda
wapi? Wanyama hawa wote mbele yako ni
mali ya nani?' 18 [n]Ndipo utakaposema, 'Ni
mali ya mtumishi wako Yakobo. Ni zawadi
ambazo zimetumwa kwa bwana wangu
Esau, naye anakuja nyuma yetu.' "

19 Akamwagiza pia yule mtumishi wa
kundi la pili, la tatu na yale mengine yote
yaliyofuata akiwaambia, "Mtamwambia
Esau maneno hayo hayo mtakapokutana
naye. 20 [o]Hakikisheni mmesema, 'Mtumishi
wako Yakobo anakuja nyuma yetu.' " Kwa
kuwa alifikiri, "Nitaweza kumtuliza kwa
zawadi hizi ninazotanguliza, hatimaye,
nitakapomwona, huenda atanikubali."

[a]2 Mahanaimu maana yake Kambi mbili.
[b]**32:3** Mwa 25:30
[c]**32:4** Mwa 18:3
[d]**32:5** Mwa 24:9; 34:11
[e]**32:6** Mwa 33:1
[f]**32:9** Mwa 31:13
[g]**32:10** Mwa 24:27
[h]**32:11** Mwa 27:41
[i]**32:12** Hos 1:10
[j]**32:13** Mwa 43:11, 15, 25, 26; Mit 18:16
[k]**32:14** Hes 7:88
[l]**32:15** Mwa 13:2
[m]**32:16** Mwa 33:8
[n]**32:18** Mwa 18:3
[o]**32:20** 1Sam 9:7

21 Kwa hiyo zawadi za Yakobo zilitangulia
mbele yake, lakini yeye mwenyewe alilala
kambini usiku ule.

*Yakobo Ashindana Mweleka Na Mungu*

22 [a]Usiku ule Yakobo akaamka
akawachukua wake zake wawili, watumishi
wake wawili wa kike na wanawe kumi na
mmoja na akavuka kivuko cha Yaboki.
23 Baada ya kuwavusha ng’ambo ya kijito,
alivusha pia mali zake zote. 24 Kwa hiyo
Yakobo akaachwa peke yake na mtu
mmoja akashikana naye mweleka mpaka
mapambazuko. 25 Yule mtu alipoona kuwa
hawezi kumshinda, aligusa kiungio cha
nyonga ya Yakobo kwa hiyo nyonga yake
ikateguka wakati alipokuwa akishikana
mweleka na yule mtu. 26 [b]Ndipo yule mtu
akasema, “Niache niende, kwa kuwa ni
mapambazuko.”

Lakini Yakobo akajibu, “Sitakuacha
uende usiponibariki.”

27 Yule mtu akamuuliza, “Jina lako nani?”

Akajibu, “Yakobo.”

28 [c]Ndipo yule mtu akasema, “Jina lako
halitakuwa tena Yakobo, bali Israeli,[d] kwa
sababu umeshindana na Mungu na watu
pia, nawe umeshinda.”

29 Yakobo akasema, “Tafadhali niambie
jina lako.”

Lakini akajibu, “Kwa nini kuniuliza Jina
langu?” Ndipo akambariki huko.

30 [e]Kwa hiyo Yakobo akapaita mahali
pale Penieli,[f] akasema, “Ni kwa sababu
nimemwona Mungu uso kwa uso na bado
maisha yangu yameokoka.”

31 [g]Jua lilikuwa linachomoza Yakobo
alipoondoka Penueli, naye alikuwa
akichechemea kwa sababu ya nyonga yake.
32 Kwa hiyo mpaka leo Waisraeli hawali
mshipa ulioungana na kiungio cha nyonga,
kwa sababu kiungio cha nyonga ya Yakobo
kiliteguliwa karibu na mshipa huo.

*Yakobo Akutana Na Esau*

33 [h]Yakobo akainua macho akamwona
Esau akija na watu wake 400, kwa
hiyo akawagawanya watoto kati ya Lea,
Raheli na wale watumishi wake wawili wa
kike. 2 Akawaweka wale watumishi wa kike
na watoto wao mbele, Lea na watoto wake
wakafuata, Raheli na Yosefu wakaja nyuma.
3 [i]Yeye mwenyewe akatangulia mbele na
kusujudu mara saba alipomkaribia ndugu
yake.

4 Lakini Esau akamkimbilia Yakobo
kumlaki na kumkumbatia, akamwangukia
shingoni na kumbusu. Nao wakalia. 5 [j]Esau
akainua macho akawaona wale wanawake
na watoto. Akauliza, “Hawa uliofuatana
nao ni nani?”

Yakobo akamjibu, “Ni watoto ambao
Mungu amempa mtumishi wako kwa
neema.”

6 Kisha wale watumishi wa kike na watoto
wao wakakaribia na kusujudu. 7 Kisha
Lea na watoto wake wakaja na kusujudu.
Mwisho wa wote wakaja Yosefu na Raheli,
nao pia wakasujudu.

8 [k]Esau akauliza, “Una maana gani kuhusu
makundi hayo yote niliyokutana nayo?”

Akasema, “Ni ili kupata kibali machoni
pako, bwana wangu.”

9 [l]Lakini Esau akamwambia, “Ndugu
yangu, tayari nina wingi wa mali. Ulivyo
navyo viwe vyako mwenyewe.”

10 [m]Yakobo akasema, “La hasha! Tafadhali,
kama nimepata kibali machoni pako,
upokee zawadi hii kutoka kwangu. Kwa
maana kuuona uso wako, ni kama kuuona
uso wa Mungu, kwa kuwa umenipokea
kwa takabali kubwa. 11 [n]Tafadhali ukubali
zawadi iliyoletwa kwako, kwa kuwa
Mungu amenineemesha na ninavyo vyote

---

[a]**32:22** Kum 2:37; 3:16
[b]**32:26** Hos 12:4
[c]**32:28** Mwa 17:5
[d]28 Israeli maana yake Yeye ashindanaye na Mungu.
[e]**32:30** Mwa 16:13
[f]30 Penieli maana yake Uso wa Mungu, ambalo ni sawa na Penueli kwa Kiebrania.
[g]**32:31** Amu 8:9
[h]**33:1** Mwa 32:6
[i]**33:3** Mwa 42:6
[j]**33:5** Za 127:3; Isa 8:18
[k]**33:8** Mwa 24:9; 32:14-16
[l]**33:9** Mwa 13:6
[m]**33:10** Mwa 16:13
[n]**33:11** 1Sam 25:27

ninavyohitaji.” Kwa sababu Yakobo
alisisitiza, Esau akapokea.
12 Ndipo Esau akasema, “Na tuendelee na
safari, nitakuwa pamoja nawe.”
13 [a]Lakini Yakobo akamwambia, “Bwana
wangu unajua kwamba watoto ni wachanga
na kwamba ni lazima nitunze hawa kondoo
wake na ng’ombe wanaonyonyesha.
Wakipelekwa kwa haraka hata kama ni
kwa siku moja tu, wanyama wote watakufa.
14 [b]Hivyo bwana wangu umtangulie
mtumishi wako, wakati mimi nikija
polepole kwa mwendo wa makundi yaliyo
mbele yangu na mwendo wa watoto, mpaka
nifike kwa bwana wangu huko Seiri.”
15 [c]Esau akamwambia, “Basi na niwaache
baadhi ya watu wangu pamoja nawe.”
Yakobo akauliza, “Lakini kwa nini ufanye
hivyo, niache tu nipate kibali machoni pa
bwana wangu.”
16 [d]Hivyo siku hiyo Esau akashika njia
akarudi Seiri. 17 [e]Pamoja na hayo, Yakobo
akaenda Sukothi,[f] mahali alipojijengea
makazi kwa ajili yake na mabanda kwa ajili
ya mifugo yake. Hii ndiyo sababu sehemu
ile inaitwa Sukothi.
18 [g]Baada ya Yakobo kutoka Padan-Aramu,
alifika salama katika mji wa Shekemu huko
Kanaani na kuweka kambi yake karibu na
mji. 19 [h]Akanunua kiwanja kutoka kwa wana
wa Hamori, baba wa Shekemu, kwa bei
ya vipande mia vya fedha, ambapo alipiga
hema lake. 20 Pale akajenga madhabahu na
kupaita El-Elohe-Israeli.[i]

*Dina Na Washekemu*

34 [j]Basi Dina, binti wa Yakobo aliyezaliwa
na Lea, akatoka nje kuwatembelea
wanawake wa nchi ile. 2 [k]Ikawa Shekemu
mwana wa Hamori Mhivi, mtawala wa
eneo lile alipomwona, akamchukua na
kumnajisi. 3 Moyo wake ukavutwa sana
kwa Dina binti Yakobo, akampenda huyu
msichana na akazungumza naye kwa
kumbembeleza. 4 [l]Shekemu akamwambia
baba yake Hamori, “Nipatie msichana huyu
awe mke wangu.”
5 [m]Yakobo aliposikia kwamba binti yake
Dina amenajisiwa, wanawe walikuwa
mashambani wakichunga mifugo yake,
kwa hiyo akalinyamazia jambo hilo mpaka
waliporudi nyumbani.
6 [n]Kisha Hamori baba yake Shekemu
akaenda kuzungumza na Yakobo. 7 [o]Basi
wana wa Yakobo walikuwa wamerudi
kutoka mashambani mara tu waliposikia
kilichotokea. Walikuwa wamejawa na
huzuni na ghadhabu, kwa sababu Shekemu
alikuwa amefanya jambo la aibu katika
Israeli kwa kukutana kimwili na binti
wa Yakobo, kitu ambacho hakingepasa
kufanyika.
8 [p]Lakini Hamori akawaambia, “Moyo
wa mwanangu Shekemu umeelekea kwa
binti yenu. Tafadhali mpeni awe mke wake.
9 [q]Oaneni na sisi, tupeni binti zenu, nanyi
mchukue binti zetu. 10 [r]Mwaweza kuishi
katikati yetu, nchi ni wazi kwenu. Ishini
ndani yake, fanyeni biashara humu na
mjipatie mali.”
11 [s]Kisha Shekemu akamwambia baba
yake Dina pamoja na ndugu zake, “Na
nipate kibali machoni penu, nami nitawapa
chochote mtakachosema. 12 [t]Niambieni kiasi
cha mahari na zawadi nitakayoileta, hata
iwe kubwa kiasi gani, nami nitawalipa
chochote mtakachodai. Nipeni tu huyu
msichana awe mke wangu.”

[a]**33:13** Isa 40:11
[b]**33:14** Kut 12:38
[c]**33:15** Mwa 32:5
[d]**33:16** Mwa 14:6
[e]**33:17** Amu 8:5, 6, 8, 14-16
[f]17 Sukothi maana yake Vibanda.
[g]**33:18** Mwa 12:6
[h]**33:19** Yos 24:32; Yn 4:5
[i]20 El-Elohe-Israeli maana yake Mungu, Mungu wa Israeli au Mwenye Nguvu ni Mungu wa Israeli.
[j]**34:1** Mwa 30:21
[k]**34:2** Mwa 33:19
[l]**34:4** Mwa 21:21
[m]**34:5** Mwa 34:2-3
[n]**34:6** Amu 14:2-5
[o]**34:7** Kum 22:21; Amu 20:6
[p]**34:8** Mwa 21:21
[q]**34:9** Kum 7:3
[r]**34:10** Mwa 47:6, 27; 13:9
[s]**34:11** Mwa 32:5
[t]**34:12** Kum 22:29; 1Sam 18:25

13 [a]Kwa sababu ndugu yao Dina alikuwa
amenajisiwa, wana wa Yakobo wakajibu
kwa udanganyifu walipozungumza na
Shekemu pamoja na baba yake Hamori.
14 [b]Wakawaambia, "Hatuwezi kufanya
jambo kama hili, hatuwezi kumtoa dada
yetu kwa mtu ambaye hakutahiriwa. Hiyo
itakuwa aibu kwetu. 15 [c]Tutakuruhusu
kwa sharti moja tu, kwamba mtakuwa
kama sisi kwa kuwatahiri wanaume wenu
wote. 16 [d]Kisha tutawapa binti zetu na sisi
tutawachukua binti zenu. Tutaishi kwenu
na tutakuwa watu wamoja nanyi. 17 Lakini
mkikataa kutahiriwa, tutamchukua ndugu
yetu na kuondoka."

18 Pendekezo lao likawa jema kwa Hamori
na Shekemu mwanawe. 19 Kijana mdogo,
ambaye alikuwa ameheshimiwa kati ya
wote walioishi nyumbani mwa baba yake,
hakupoteza muda kufanya waliyoyasema,
kwa sababu alikuwa amependezwa sana
na binti Yakobo. 20 [e]Kwa hiyo Hamori na
Shekemu mwanawe walikwenda kwenye
lango la mji kuzungumza na wenzao
wa mjini. 21 [f]Wakasema, "Hawa watu ni
marafiki kwetu, tuwaruhusu waishi katika
nchi yetu na kufanya biashara ndani yake,
nchi ina nafasi tele kwa ajili yao. Tunaweza
kuoa binti zao. Nao wanaweza kuoa binti
zetu. 22 [g]Lakini watu hao watakuwa tayari
kukubali kuishi nasi kama watu wamoja
nao kwa sharti kwamba wanaume wetu
watahiriwe, kama wao. 23 [h]Je, si mifugo yao,
mali zao na wanyama wao wengine wote
watakuwa wetu? Basi na tuwape kibali, nao
wataishi miongoni mwetu."

24 [i]Wanaume wote waliotoka nje ya lango
la mji walikubaliana na Hamori na Shekemu
mwanawe na kila mwanaume katika mji ule
akatahiriwa.

25 [j]Baada ya siku tatu, wakati wote
wakiwa wangali katika maumivu, wana
wawili wa Yakobo, yaani Simeoni na Lawi,
ndugu zake Dina, wakachukua panga zao
na kuvamia mji ambao haukutazamia vita,
wakaua kila mwanaume. 26 Wakawaua
Hamori na Shekemu mwanawe kwa
upanga kisha wakamchukua Dina kutoka
nyumba ya Shekemu na kuondoka. 27 Wana
wa Yakobo walipita juu ya maiti katika
kuteka nyara mji ule ambamo dada yao
alikuwa amenajisiwa. 28 Wakachukua
kondoo na mbuzi, ng'ombe, punda na
kila kitu kilichokuwa chao ndani ya mji
ule na mashambani. 29 Walichukua utajiri
wao wote pamoja na wanawake na watoto
wao, wakachukua nyara kila kitu ndani ya
nyumba zao.

30 Kisha Yakobo akawaambia Simeoni
na Lawi, "Mmeleta taabu kwangu kwa
kunifanya ninuke kama uvundo kwa
Wakanaani na Waperizi, watu waishio
katika nchi hii. Sisi ni wachache, kama
wakiunganisha nguvu zao dhidi yangu na
kunishambulia, mimi na nyumba yangu
tutaangamizwa."

31 Lakini wakamjibu, "Je, ilikuwa vyema
kumtendea dada yetu kama kahaba?"

*Yakobo Arudi Betheli*

35 [k]Kisha Mungu akamwambia Yakobo,
"Panda uende Betheli ukakae huko na
ukamjengee Mungu madhabahu huko, Yeye
aliyekutokea ulipokuwa unamkimbia Esau
ndugu yako."

2 [l]Hivyo Yakobo akawaambia watu
wa nyumbani mwake pamoja na wote
waliokuwa naye, "Iondoeni miungu ya
kigeni ile iliyoko katikati yenu, jitakaseni
na mkabadilishe nguo zenu. 3 [m]Kisha njooni,
twende Betheli, mahali nitakapomjengea
Mungu madhabahu, aliyenijibu katika
siku ya shida yangu, ambaye amekuwa
pamoja nami popote nilipokwenda."
4 [n]Kwa hiyo wakampa Yakobo miungu yote

[a]**34:13** Mwa 27:36
[b]**34:14** Mwa 17:14; Isa 31:4
[c]**34:15** 1Sam 11:2; Kut 12:48
[d]**34:16** Mwa 33:19
[e]**34:20** Mwa 18:1
[f]**34:21** Mwa 33:19
[g]**34:22** Mwa 34:15
[h]**34:23** Mwa 34:28
[i]**34:24** Mwa 18:1
[j]**34:25** Mwa 49:5; 49:7
[k]**35:1** Mwa 12:8
[l]**35:2** Yos 24:15; Kut 19:10, 14
[m]**35:3** Mwa 32:7; Amu 2:15
[n]**35:4** Mwa 24:22

ya kigeni waliyokuwa nayo, pamoja na
pete zilizokuwa masikioni mwao. Yakobo
akavizika chini ya mti wa mwaloni huko
Shekemu. 5 [a]Kisha wakaondoka, na hofu ya
Mungu ikawapata miji yote iliyowazunguka.
Kwa hiyo hakuna aliyewafuatia wana wa
Yakobo.

6 [b]Yakobo na watu wote waliokuwa
pamoja naye wakafika Luzu (ndio Betheli),
katika nchi ya Kanaani. 7 [c]Huko akajenga
madhabahu na akapaita mahali pale
El-Betheli,[d] kwa sababu mahali pale ndipo
Mungu alipojifunua kwake alipokuwa
akimkimbia ndugu yake.

8 [e]Wakati huu Debora, mlezi wa Rebeka,
akafa na akazikwa chini ya mti wa mwaloni
ulioko chini ya Betheli. Kwa hiyo pakaitwa
Alon-Bakuthi.[f]

9 [g]Baada ya Yakobo kurudi kutoka
Padan-Aramu, Mungu alimtokea tena
na kumbariki. 10 [h]Mungu akamwambia,
"Jina lako ni Yakobo, lakini hutaitwa tena
Yakobo, jina lako utakuwa Israeli." Kwa
hiyo akamwita Israeli.

11 [i]Mungu akamwambia, "Mimi ndimi
Mungu Mwenyezi,[j] ukazae na kuongezeka.
Taifa na jamii ya mataifa itatoka kwako,
nao wafalme watatoka viunoni mwako.
12 [k]Nchi niliyowapa Abrahamu na Isaki
nakupa wewe pia, nami nitawapa wazao
wako baada yako." 13 [l]Kisha Mungu
akapanda juu kutoka kwake mahali pale
alipozungumza naye.

14 [m]Yakobo akasimamisha nguzo ya jiwe
mahali pale Mungu alipozungumza naye,
akamimina sadaka ya kinywaji juu yake,
pia akamimina mafuta juu yake. 15 [n]Yakobo
akapaita mahali pale Mungu alipozungumza
naye Betheli.[o]

*Vifo Vya Raheli Na Isaki*

16 [p]Kisha wakaondoka Betheli.
Walipokuwa umbali fulani kabla ya kufika
Efrathi, Raheli akaanza kusikia uchungu
na alipata shida kuu. 17 [q]Alipokuwa katika
shida hii katika kujifungua, mkunga
akamwambia, "Usiogope, kwa sababu
umempata mwana mwingine." 18 [r]Hapo
alipopumua pumzi yake ya mwisho,
kwa maana alikuwa akifa, akamwita
mwanawe Benoni.[s] Lakini babaye akamwita
Benyamini.[t]

19 [u]Kwa hiyo Raheli akafa, akazikwa
kando ya njia iendayo Efrathi (ndio
Bethlehemu). 20 [v]Juu ya kaburi lake, Yakobo
akasimamisha nguzo, ambayo mpaka leo
inatambulisha kaburi la Raheli.

21 Israeli akaendelea tena na safari yake
na kupiga hema mbele mnara wa Ederi.
22 Wakati Israeli alipokuwa akiishi katika
nchi ile, Reubeni mwanawe alikutana
kimwili na suria wa baba yake aitwaye
Bilha, naye Israeli akasikia jambo hili.

Yakobo alikuwa na wana kumi na wawili:

23 Wana wa Lea walikuwa:
Reubeni mzaliwa wa kwanza wa Yakobo,
Simeoni, Lawi, Yuda, Isakari na Zabuloni.
24 [w]Wana wa Raheli walikuwa:
Yosefu na Benyamini.
25 [x]Wana waliozaliwa na Bilha

[a]**35:5** Kut 15:16
[b]**35:6** Mwa 28:19; 10:19
[c]**35:7** Mwa 8:20
[d]7 El-Betheli maana yake Mungu wa Betheli.
[e]**35:8** Mwa 24:59; 12:8
[f]8 Alon-Bakuthi maana yake Mwaloni wa Kilio.
[g]**35:9** Mwa 28:13; 32:29
[h]**35:10** Mwa 17:5
[i]**35:11** Mwa 17:1; 17:6
[j]11 Mungu Mwenyezi hapa ni jina la Kiebrania, El-Shaddai (yaani Mungu Mwenye utoshelevu wote).
[k]**35:12** Mwa 28:13; 12:7
[l]**35:13** Mwa 17:22
[m]**35:14** Mwa 28:18; Kut 29:40
[n]**35:15** Mwa 12:8
[o]15 Betheli maana yake Nyumba ya Mungu.
[p]**35:16** Mwa 48:7
[q]**35:17** Kut 1:15; Mwa 30:24
[r]**35:18** 1Sam 4:21
[s]18 Benoni maana yake Mwana wa huzuni yangu.
[t]18 Benyamini maana yake Mwana wa mkono wangu wa kuume.
[u]**35:19** Mwa 48:7
[v]**35:20** 1Sam 10:2; 6:18
[w]**35:24** Mwa 30:24; 35:18
[x]**35:25** Mwa 30:24

mtumishi wa kike wa Raheli
walikuwa:
Dani na Naftali.
26 [a]Wana waliozaliwa na Zilpa
mtumishi wa kike wa Lea
walikuwa:
Gadi na Asheri.

Hawa walikuwa wana wa Yakobo, waliozaliwa kwake akiwa Padan-Aramu.

27 [b]Yakobo akarudi nyumbani kwa
baba yake Isaki huko Mamre, karibu na
Kiriath-Arba (yaani Hebroni), ambapo
walikuwa wameishi Abrahamu na Isaki.
28 [c]Isaki aliishi miaka 180. 29 [d]Kisha Isaki
akapumua pumzi yake ya mwisho akafa,
akakusanywa pamoja na watu wake akiwa
mzee wa miaka mingi. Nao wanawe Esau
na Yakobo wakamzika.

*Wazao Wa Esau*

**(1 Nyakati 1:34-42)**

36 [e]Hivi ndivyo vizazi vya Esau (yaani
Edomu).

2 [f]Esau akaoa wake kutoka miongoni
mwa wanawake wa Kanaani: Ada
binti wa Eloni Mhiti, Oholibama binti
wa Ana, mjukuu wa kike wa Sibeoni
Mhivi, 3 pia akaoa Basemathi binti wa
Ishmaeli, dada yake Nebayothi.
4 [g]Ada akamzalia Esau Elifazi,
Basemathi akamzaa Reueli,
5 [h]Oholibama akamzaa Yeushi, Yalamu
na Kora. Hawa ndio wana wa Esau
waliozaliwa kwake huko Kanaani.
6 [i]Esau akawachukua wake zake,
watoto wake wa kiume na wa kike na
wote wa nyumbani mwake, mifugo
yake pamoja na wanyama wake
wengine wote na mali yake yote
ambayo alikuwa ameipata akiwa
Kanaani, akahamia katika nchi iliyo
mbali na Yakobo ndugu yake. 7 [j]Mali
zao zilikuwa nyingi sana kiasi kwamba
haikuwa rahisi wao kuishi pamoja, nchi
waliyokuwa wakiishi isingewatosha
wote kwa ajili ya mifugo yao. 8 [k]Kwa
hiyo Esau (ambaye ni Edomu) aliishi
katika nchi ya kilima huko Seiri.

9 [l]Hawa ndio wazao wa Esau, baba wa
Waedomu, katika nchi ya kilima cha Seiri.

10 [m]Haya ndiyo majina ya wana wa
Esau:
Elifazi, mwana wa Esau ambaye
mkewe Ada alimzalia; na Reueli,
mwana wa Esau ambaye mkewe
Basemathi alimzalia.
11 [n]Wana wa Elifazi ni:
Temani, Omari, Sefo, Gatamu na
Kenazi.
12 [o]Elifazi mwana wa Esau alikuwa
pia na suria aliyeitwa Timna,
ambaye alimzalia Amaleki. Hawa
ndio waliokuwa wajukuu wa Ada
mke wa Esau.
13 [p]Wana wa Reueli ni:
Nahathi, Zera, Shama na Miza.
Hawa ndio waliokuwa wajukuu
wa Basemathi mkewe Esau.
14 [q]Wana wa Oholibama binti Ana,
mkewe Esau, aliyekuwa mjukuu wa
Sibeoni, aliomzalia Esau ni:
Yeushi, Yalamu na Kora.

15 [r]Hawa ndio waliokuwa wakuu
miongoni mwa wazao wa Esau:

Wakuu wa wana wa Elifazi, mzaliwa
wa kwanza wa Esau ni:
Temani, Omari, Sefo, Kenazi,
16 [s]Kora, Gatamu na Amaleki.
Hawa ndio waliokuwa wakuu

[a]**35:26** Mwa 37:2
[b]**35:27** Mwa 13:18; Amu 1:10
[c]**35:28** Mwa 25:7
[d]**35:29** Mwa 15:15; 25:8-9
[e]**36:1** Mwa 2:4; 25:30
[f]**36:2** Mwa 26:34; 28:8-9
[g]**36:4** 1Nya 1:35
[h]**36:5** 1Nya 1:35
[i]**36:6** Mwa 12:5; 1Nya 1:35
[j]**36:7** Mwa 13:6; 27:39
[k]**36:8** Kum 2:4
[l]**36:9** Mwa 2:4
[m]**36:10** Mwa 36:3
[n]**36:11** 1Nya 1:45
[o]**36:12** Kut 17:8, 16; 1Sam 15:2
[p]**36:13** Mwa 36:3
[q]**36:14** Mwa 36:2
[r]**36:15** Mwa 36:19-40; Kut 15:15
[s]**36:16** Mwa 32:3

waliotoka kwa Elifazi huko
Edomu, waliokuwa wajukuu wa
kiume wa Ada.
17 [a]Wakuu wa wana wa Reueli, mwana
wa Esau ni:
Nahathi, Zera, Shama na Miza.
Hawa ndio wakuu waliotoka kwa
Reueli huko Edomu, waliokuwa
wajukuu wa kiume wa Basemathi
mkewe Esau.
18 [b]Wakuu wa wana wa Esau ambao
mkewe Oholibama alimzalia ni:
Yeushi, Yalamu na Kora. Hawa
ndio wakuu waliotoka kwa mke
wa Esau, Oholibama binti Ana.

19 [c]Hawa ndio waliokuwa wana wa Esau (ndiye Edomu), na hawa ndio waliokuwa wakuu wao.

20 [d]Hawa ndio walikuwa wana wa Seiri, Mhori, waliokuwa wakiishi katika nchi ile:

Lotani, Shobali, Sibeoni, Ana,
21 [e]Dishoni, Eseri na Dishani. Hawa
ndio wana wa Seiri huko Edomu
waliokuwa wakuu kwa Wahori.
22 Wana wa Lotani walikuwa:
Hori na Homamu. Timna alikuwa
dada yake Lotani.
23 Wana wa Shobali walikuwa:
Alvani, Manahathi, Ebali, Shefo na
Onamu.
24 [f]Wana wa Sibeoni walikuwa:
Aiya na Ana. Huyu Ana ndiye
aligundua chemchemi ya maji
moto jangwani alipokuwa
akichunga punda za Sibeoni baba
yake.
25 [g]Watoto wa Ana walikuwa:
Dishoni na Oholibama binti wa
Ana.
26 Wana wa Dishoni walikuwa:
Hemdani, Eshbani, Ithrani na
Kerani.
27 Wana wa Eseri walikuwa:
Bilhani, Zaavani na Akani.
28 Wana wa Dishani walikuwa:
Usi na Arani.
29 [h]Hawa ndio waliokuwa wakuu wa
Wahori:
Lotani, Shobali, Sibeoni, Ana,
30 [i]Dishoni, Eseri na Dishani. Hawa
ndio walikuwa wakuu wa Wahori,
kufuatana na makundi yao, katika
nchi ya Seiri.

*Watawala Wa Edomu*

**(1 Nyakati 1:43-54)**

31 [j]Wafuatao ni wafalme waliotawala
Edomu kabla ya mfalme yeyote wa Israeli
kutawala:

32 Bela mwana wa Beori alikuwa
mfalme wa Edomu. Mji wake
uliitwa Dinhaba.
33 [k]Bela alipofariki, Yobabu mwana wa
Zera kutoka Bosra akawa mfalme
baada yake.
34 [l]Yobabu alipofariki, Hushamu kutoka
nchi ya Watemani akawa mfalme
baada yake.
35 [m]Hushamu alipofariki, Hadadi
mwana wa Bedadi, aliyeshinda
Midiani katika nchi ya Moabu,
akawa mfalme baada yake. Mji
wake uliitwa Avithi.
36 Hadadi alipofariki, Samla kutoka
Masreka akawa mfalme baada
yake.
37 [n]Samla alipofariki, Shauli kutoka
Rehobothi ng’ambo ya Mto Frati
akawa mfalme baada yake.
38 Shauli alipofariki, Baal-Hanani
mwana wa Akbori akawa mfalme
baada yake.
39 Baal-Hanani mwana wa Akbori
alipofariki, Hadadi akawa mfalme

[a] **36:17** 1Nya 1:37
[b] **36:18** Mwa 36:2
[c] **36:19** 1Nya 1:35
[d] **36:20** Mwa 14:6
[e] **36:21** Mwa 36:30
[f] **36:24** Mwa 36:2
[g] **36:25** Mwa 36:2
[h] **36:29** Mwa 36:20
[i] **36:30** Mwa 36:21
[j] **36:31** Mwa 17:6
[k] **36:33** Isa 34:6
[l] **36:34** Yer 49:7
[m] **36:35** Rut 1:1, 6; Mwa 19:37
[n] **36:37** Mwa 26:22

baada yake. Mji wake uliitwa Pau,
na mkewe aliitwa Mehetabeli binti
Matredi, binti Me-Zahabu.

40 [a]Hawa ndio wakuu waliotokana na
Esau, kwa majina, kufuatana na koo zao
na nchi zao:

Timna, Alva, Yethethi,
41 Oholibama, Ela, Pinoni,
42 Kenazi, Temani, Mibsari,
43 [b]Magdieli na Iramu. Hawa ndio
walikuwa wakuu wa Edomu,
kufuatana na makazi yao katika
nchi waliyoimiliki.

Huyu ndiye alikuwa Esau, baba wa
Waedomu.

*Ndoto Za Yosefu*

37 [c]Yakobo akaishi Kanaani katika nchi
ambayo baba yake alikuwa ameishi.

2 [d]Zifuatazo ni habari za Yakobo.

Yosefu, kijana wa miaka kumi na saba,
alikuwa akichunga makundi ya kondoo na
mbuzi pamoja na ndugu zake wa mama
wengine, yaani wana wa Bilha na wana
wa Zilpa wake za baba yake, naye akawa
akimletea baba yake taarifa mbaya kuhusu
hao ndugu zake.
3 [e]Basi, Israeli akampenda Yosefu kuliko
yeyote miongoni mwa kaka zake, kwani
ni mwanawe wa uzeeni, akamshonea joho
lililorembwa vizuri sana. 4 [f]Ndugu zake
walipoona kwamba baba yao anampenda
Yosefu kuliko yeyote mwingine miongoni
mwao, walimchukia na hawakusema naye
neno lolote jema.
5 Yosefu akaota ndoto, naye alipowaeleza
ndugu zake, wakamchukia zaidi.
6 Akawaambia, "Sikilizeni ndoto niliyoota:
7 [g]Tulikuwa tukifunga miganda ya nafaka
shambani, ghafula mganda wangu
ukasimama wima, wakati miganda yenu
ikiuzunguka na kuuinamia."
8 [h]Ndugu zake wakamwambia, "Wewe
unakusudia kututawala? Hivi kweli wewe
utatutawala sisi?" Wakaongeza kumchukia
zaidi kwa sababu ya ndoto yake pamoja na
yale aliyowaambia.
9 Kisha akaota ndoto nyingine,
akawaambia ndugu zake akisema,
"Sikilizeni, nimeota ndoto nyingine, wakati
huu jua, mwezi na nyota kumi na moja
zilikuwa zinanisujudia."
10 [i]Alipomwambia baba yake pamoja
na ndugu zake, baba yake akamkemea
akisema, "Ni ndoto gani hii uliyoota? Hivi
kweli mama yako na mimi na ndugu zako
tutakuja kukusujudia wewe hadi nchi?"
11 [j]Ndugu zake wakamwonea wivu, lakini
baba yake akaliweka jambo hilo moyoni.

*Yosefu Auzwa Na Ndugu Zake*

12 [k]Basi, ndugu zake walikuwa
wamekwenda kuchunga makundi ya baba
yao karibu na Shekemu, 13 [l]naye Israeli
akamwambia Yosefu, "Kama ujuavyo,
ndugu zako wanachunga makundi huko
karibu na Shekemu. Njoo, nitakutuma
kwao."
Yosefu akajibu, "Vema sana, niko tayari."
14 [m]Kwa hiyo akamwambia, "Nenda uone
kama mambo yote ni salama kwa ndugu
zako na makundi, kisha uniletee habari."
Ndipo akamtuma Yosefu kutoka Bonde la
Hebroni.
Yosefu alipofika Shekemu, 15 mtu mmoja
akamkuta akizungukazunguka mashambani
na akamuuliza, "Unatafuta nini?"
16 Akajibu, "Ninawatafuta ndugu zangu.
Unaweza kuniambia wanachunga wapi
makundi yao?"
17 [n]Yule mtu akajibu, "Wamehama hapa.
Nilisikia wakisema, 'Twende Dothani.' "
Kwa hiyo Yosefu akawafuatilia ndugu

[a]**36:40** Mwa 36:15
[b]**36:43** Mwa 36:9
[c]**37:1** Mwa 17:8; 10:19
[d]**37:2** Za 78:71; 1Sam 2:24
[e]**37:3** Mwa 44:20; 2Sam 13:18-19
[f]**37:4** Mwa 27:41; Mdo 7:9
[g]**37:7** Mwa 42:6, 9; 43:26, 28
[h]**37:8** Mwa 49:26; Kum 33:16
[i]**37:10** Rut 2:16
[j]**37:11** Mdo 7:9; Lk 2:19, 51
[k]**37:12** Mwa 12:6
[l]**37:13** Mwa 17:5
[m]**37:14** 1Sam 17:18
[n]**37:17** 2Fal 6:13

zake na kuwakuta karibu na Dothani.
18 [a]Ndugu zake walipomwona akiwa mbali,
kabla hajawafikia, wakapanga shauri baya
la kumuua.
19 [b]Wakaambiana, “Yule mwota ndoto
anakuja! 20 [c]Njooni sasa, tumuue na
kumtupa katika shimo mojawapo na tuseme
kwamba mnyama mkali amemrarua. Kisha
tutaona matokeo ya ndoto zake.”
21 [d]Reubeni aliposikia jambo hili,
akajaribu kumwokoa kutoka mikononi
mwao akasema, “Tusiutoe uhai wake.
22 [e]Tusimwage damu yoyote. Mtupeni
katika shimo lililoko hapa jangwani,
lakini msimguse.” Reubeni alisema hivyo
ili amwokoe kutoka mikononi mwao, kisha
amrudishe nyumbani kwa baba yake.
23 [f]Kwa hiyo Yosefu alipowafikia ndugu
zake, walimvua lile joho lake, lile joho
lililorembwa vizuri alilokuwa amevaa.
24 [g]Kisha wakamchukua wakamtupa katika
shimo. Wakati huo shimo lilikuwa tupu,
halikuwa na maji ndani yake.
25 [h]Walipokaa ili wale chakula chao,
wakainua macho wakaona msafara wa
Waishmaeli ukija kutoka Gileadi. Ngamia
wao walikuwa wamepakizwa mizigo ya
vikolezo, uvumba na manemane, nao
walikuwa njiani kuvipeleka Misri.
26 [i]Yuda akawaambia ndugu zake,
“Tutafaidi nini ikiwa tutamuua ndugu yetu
na kuificha damu yake? 27 [j]Njooni, tumuuze
kwa hawa Waishmaeli. Tusimguse, kwa
kuwa hata hivyo yeye ni ndugu yetu, nyama
yetu na damu yetu wenyewe.” Ndugu zake
wakakubali.
28 [k]Kwa hiyo wale wafanyabiashara
Wamidiani walipofika pale, ndugu zake
wakamtoa Yosefu kutoka kwenye lile
shimo, na kumuuza kwa shekeli ishirini[l]
za fedha kwa wale Waishmaeli, ambao
walimpeleka Misri.
29 [m]Reubeni aliporudi kutazama kwenye
lile shimo na kuona kwamba Yosefu
hayupo, alirarua nguo zake. 30 [n]Akawarudia
ndugu zake na kusema, “Kijana hayuko
mle! Nielekee wapi sasa?”
31 Kisha wakalichukua lile joho la
Yosefu, wakachinja mbuzi na kulichovya
katika damu. 32 Wakalichukua lile joho
lililorembwa vizuri na kulipeleka kwa baba
yao na kusema, “Tumeliokota hili joho.
Uchunguze uone kama ni la mwanao.”
33 [o]Baba yao akalitambua akasema, “Hili
ni joho la mwanangu! Mnyama mkali
amemrarua. Hakika Yosefu ameraruliwa
vipande vipande.”
34 [p]Kisha Yakobo akararua nguo zake,
akavaa nguo ya gunia na kumwombolezea
mwanawe kwa siku nyingi. 35 [q]Wanawe
wote na binti zake wakaja kumfariji, lakini
hakukubali kufarijiwa. Akasema, “Hapana,
nitamwombolezea mwanangu mpaka
nimfikie kaburini.” Kwa hiyo baba yake
akaendelea kumlilia.
36 [r]Wakati ule ule, Wamidiani wakamuuza
Yosefu huko Misri kwa Potifa, mmojawapo
wa maafisa wa Farao, aliyekuwa mkuu wa
ulinzi.

### *Yuda Na Tamari*

38 [s]Wakati ule, Yuda akawaacha
ndugu zake, akaenda kuishi na Hira
Mwadulami. 2 [t]Huko Yuda akakutana na
binti wa Kikanaani aitwaye Shua, akamwoa
na akakutana naye kimwili, 3 [u]akapata
mimba, akamzaa mwana, ambaye alimwita
Eri. 4 Akapata mimba tena, akamzaa mwana

[a]**37:18** Mk 14:1
[b]**37:19** Mwa 28:12
[c]**37:20** Mwa 50:20
[d]**37:21** Mwa 42:22
[e]**37:22** Mwa 37:20
[f]**37:23** Mwa 37:3
[g]**37:24** Mwa 37:4
[h]**37:25** Mwa 37:28
[i]**37:26** Mwa 4:10
[j]**37:27** Mwa 42:21
[k]**37:28** Kut 21:16; Za 105:17

[l]28 Shekeli 20 ni sawa na gramu 200.
[m]**37:29** Ay 1:20; Yoe 2:13
[n]**37:30** Mwa 37:22
[o]**37:33** Mwa 37:20
[p]**37:34** 2Sam 3:31; 2Fal 6:30; Ay 16:15
[q]**37:35** Mwa 42:38; 2Sam 12:23
[r]**37:36** Mwa 39:1; 1Sam 22:14
[s]**38:1** Yos 12:15; 2Nya 11:7
[t]**38:2** 1Nya 2:3
[u]**38:3** Mwa 38:6; Hes 26:19

na kumwita Onani. 5 [a]Akamzaa mwana
mwingine tena, akamwita Shela. Huyu
alimzalia mahali paitwapo Kezibu.
6 Yuda akampatia Eri, mzaliwa wake
wa kwanza, mke aitwaye Tamari. 7 [b]Lakini
Eri, mzaliwa wa kwanza wa Yuda, alikuwa
mwovu machoni pa BWANA, kwa hiyo
BWANA akamuua.
8 [c]Kisha Yuda akamwambia Onani,
“Kutana kimwili na mke wa ndugu yako,
na utimize wajibu wako kwake kama mke
wa ndugu yako, ili umpatie ndugu yako
uzao.” 9 Lakini Onani alijua kwamba
uzao haungekuwa wake, kwa hiyo kila
alipokutana kimwili na mke wa ndugu
yake, alimwaga chini mbegu za kiume ili
asimpatie ndugu yake uzao. 10 Alichofanya
kilikuwa kiovu machoni pa BWANA, hivyo,
pia BWANA akamuua Onani.
11 [d]Kisha Yuda akamwambia Tamari
mkwewe, “Ishi kama mjane nyumbani
mwa baba yako mpaka mwanangu
Shela atakapokua.” Kwa maana alifikiri,
“Angeweza kufa pia kama ndugu zake.” Kwa
hiyo Tamari alikwenda kuishi nyumbani
kwa baba yake.
12 Baada ya muda mrefu mke wa
Yuda binti wa Shua akafariki. Baada
ya msiba, Yuda alikwenda Timna, kwa
watu waliokuwa wakikata kondoo wake
manyoya, naye alifuatana na rafiki yake
Hira Mwadulami.
13 Tamari alipoambiwa, “Baba mkwe
wako yuko njiani kwenda Timna kukata
kondoo wake manyoya,” 14 [e]alivua mavazi
yake ya ujane, akajifunika kwa shela ili
asifahamike, akaketi kwenye mlango wa
Enaimu, ambao upo njiani kuelekea Timna.
Akafanya hivyo kwa sababu aliona kwamba,
ingawa Shela amekua, lakini alikuwa
hajakabidhiwa kwake kuwa mkewe.
15 [f]Yuda alipomwona alifikiri ni kahaba,
kwa sababu alikuwa amefunika uso wake.
16 Pasipo kutambua kwamba alikuwa
mkwe wake, akamwendea kando ya njia
na kumwambia, “Njoo sasa, nikutane na
wewe kimwili.”
Yule mkwewe akamuuliza, “Utanipa nini
nikikutana nawe kimwili?”
17 [g]Akamwambia, “Nitakutumia mwana-
mbuzi kutoka kundi langu.”
Akamuuliza, “Utanipa kitu chochote
kama amana mpaka utakapompeleka?”
18 [h]Akamuuliza, “Nikupe amana gani?”
Akamjibu, “Pete yako na kamba yake
pamoja na fimbo iliyo mkononi mwako.”
Kwa hiyo akampa vitu hivyo kisha
akakutana naye kimwili, naye akapata
mimba yake. 19 [i]Tamari akaondoka, akavua
shela yake akavaa tena nguo zake za ujane.
20 Wakati ule ule, Yuda akamtuma rafiki
yake Mwadulami apeleke yule mwana-
mbuzi ili arudishiwe amana yake kutoka
kwa yule mwanamke, lakini yule rafiki yake
hakumkuta yule mwanamke. 21 [j]Akawauliza
watu wanaoishi mahali pale, “Yuko wapi
yule kahaba wa mahali pa kuabudia
miungu aliyekuwa kando ya barabara hapa
Enaimu?”
Wakamjibu, “Hajawahi kuwepo
mwanamke yeyote kahaba wa mahali pa
kuabudia miungu hapa.”
22 Kwa hiyo akamrudia Yuda na
kumwambia, “Sikumpata. Zaidi ya hayo,
watu wanaoishi mahali pale walisema
‘Hapakuwahi kuwepo mwanamke yeyote
kahaba wa mahali pa kuabudia miungu
hapa.’ ”
23 [k]Kisha Yuda akasema, “Mwache
avichukue vitu hivyo, ama sivyo tutakuwa
kichekesho. Hata hivyo, nilimpelekea
mwana-mbuzi, lakini hukumkuta.”
24 [l]Baada ya miezi mitatu Yuda
akaambiwa, “Tamari mkweo ana hatia
ya kuwa kahaba, na matokeo yake ana
mimba.”
Yuda akasema, “Mtoeni nje na achomwe
moto hadi afe!”

---

[a]**38:5** Hes 26:20
[b]**38:7** Mwa 46:12
[c]**38:8** 1Nya 2:3
[d]**38:11** Rut 1:13
[e]**38:14** Mwa 24:65
[f]**38:15** Amu 11:1
[g]**38:17** Mwa 38:20
[h]**38:18** 1Fal 21:8; Isa 49:16
[i]**38:19** Mwa 38:14
[j]**38:21** Law 19:29; 2Fal 23:7
[k]**38:23** Ay 12:3; Yer 20:7
[l]**38:24** Yos 7:25; 1Sam 31:12

25 Alipokuwa akitolewa nje, akatuma ujumbe kwa baba mkwe wake kusema, “Nina mimba ya mtu mwenye vitu hivi.” Akaongeza kusema, “Angalia kama utatambua kwamba pete hii na kamba yake pamoja na fimbo hii ni vya nani.”

26 [a]Yuda akavitambua na kusema, “Yeye ana haki kuliko mimi, kwa kuwa sikumkabidhi kwa mwanangu Shela ili awe mkewe.” Tangu hapo hakukutana naye kimwili tena.

27 Wakati ulipofika wa kujifungua, kukawa na wana mapacha tumboni mwake. 28 Alipokuwa akijifungua, mmoja akatoa mkono wake nje, kwa hiyo mkunga akachukua uzi mwekundu na kuufunga mkononi mwa yule mtoto, akasema, “Huyu ametoka kwanza.” 29 [b]Lakini alipourudisha mkono wake ndugu yake akaanza kutoka, naye akasema, “Hivi ndivyo ulivyotoka kwa nguvu!” Akaitwa Peresi. 30 Kisha ndugu yake, aliyekuwa na uzi mwekundu mkononi, akatoka, naye akaitwa Zera.

### *Yosefu Na Mke Wa Potifa*

39 [c]Wakati huu Yosefu alikuwa amechukuliwa mpaka Misri. Mmisri aliyeitwa Potifa aliyekuwa mmojawapo wa maafisa wa Farao, mkuu wa ulinzi, akamnunua Yosefu kutoka kwa Waishmaeli waliomleta Misri.

2 Bwana alikuwa pamoja na Yosefu, naye akastawi, Yosefu akaishi nyumbani kwa bwana wake Mmisri. 3 [d]Potifa alipoona kuwa Bwana alikuwa pamoja na Yosefu na kwamba Bwana alimfanikisha kwa kila kitu alichokifanya, 4 [e]Yosefu alipata kibali machoni pa Potifa, akamfanya mhudumu wake. Potifa akamweka kuwa msimamizi wa nyumba yake, naye akamkabidhi kuwa mwangalizi wa kila kitu alichokuwa nacho. 5 [f]Kuanzia wakati huo Potifa alipomweka Yosefu kuwa msimamizi wa nyumba na mali zake zote alizokuwa nazo, Bwana aliibariki nyumba ya Mmisri huyo kwa sababu ya Yosefu. Baraka ya Bwana ilikuwa juu ya kila kitu alichokuwa nacho Potifa, nyumbani na shambani. 6 Kwa hiyo Potifa akamwachia Yosefu uangalizi wa kila kitu alichokuwa nacho, Yosefu alipokuwa katika uongozi, Potifa hakuwa na sababu ya kujishughulisha na kitu chochote isipokuwa chakula alichokula.

Yosefu alikuwa mwenye umbo zuri na sura ya kuvutia; 7 baada ya kitambo mke wa Potifa akamtamani Yosefu, akamwambia, “Njoo, ukutane nami kimwili!”

8 [g]Lakini Yosefu akakataa. Akamwambia yule mwanamke, “Mimi nikiwa katika uongozi, bwana wangu hahusiki na kitu chochote katika nyumba hii, kila kitu alicho nacho amenikabidhi. 9 [h]Hapa nyumbani hakuna aliye mkuu kuliko mimi. Bwana wangu hakunizuilia kitu chochote isipokuwa wewe, kwa kuwa wewe ni mke wake. Nitawezaje basi kufanya uovu huu na kutenda dhambi dhidi ya Mungu?” 10 Ingawa yule mwanamke aliendelea kumshawishi Yosefu siku baada ya siku, Yosefu alikataa kukutana naye kimwili wala kukaa karibu naye.

11 [i]Siku moja Yosefu akaingia ndani ya nyumba kufanya kazi zake, wala hapakuwepo na mfanyakazi yeyote ndani ya nyumba. 12 [j]Mke wa Potifa akashika vazi Yosefu alilokuwa amevaa, akamwambia, “Njoo tukutane kimwili!” Lakini Yosefu akaacha vazi lake mkononi mwa huyo mwanamke, akatoka nje ya nyumba akikimbia.

13 Yule mwanamke alipoona kwamba Yosefu amemwachia vazi lake mkononi na kukimbilia nje ya nyumba, 14 [k]akawaita watumishi wake wa nyumbani, akawaambia, “Tazameni! Huyu Mwebrania ameletwa hapa kutudhihaki! Aliingia hapa ndani ili akutane nami kimwili, lakini nikapiga kelele. 15 Aliposikia kelele za kuomba

[a]**38:26** 1Sam 24:17; Mwa 38:11
[b]**38:29** Hes 26:20-21; Mt 1:3
[c]**39:1** Mwa 37:36
[d]**39:3** Mwa 21:22; Za 1:3
[e]**39:4** 1Fal 11:28
[f]**39:5** 2Sam 6:11; Za 128:4
[g]**39:8** Mit 6:23-24
[h]**39:9** Hes 22:34
[i]**39:11** Kut 18:20
[j]**39:12** Mit 7:13; 2Tim 2:22
[k]**39:14** Kum 22:24, 27

msaada, akaacha vazi lake kando yangu
akakimbilia nje.”
16 Yule mwanamke akaliweka lile vazi
karibu naye mpaka Potifa aliporudi
nyumbani. 17 [a]Ndipo akamweleza kisa hiki,
akisema: “Yule mtumwa wa Kiebrania
uliyetuletea alinijia ili kunidhihaki.
18 Lakini mara nilipopiga kelele kuomba
msaada, akaliacha vazi lake kando yangu
akakimbia nje ya nyumba.”
19 Potifa aliposikia kisa hiki mkewe
alichomweleza, akisema, “Hivi ndivyo
mtumwa wako alivyonitenda.” Hasira ya
Potifa ikawaka. 20 [b]Potifa akamchukua
Yosefu na kumweka gerezani, mahali
ambapo wahalifu wa mfalme walikuwa
wamefungwa.
Lakini wakati Yosefu alipokuwa huko
gerezani, 21 [c]BWANA alikuwa pamoja
naye, akamhurumia na kumpa kibali
mbele ya msimamizi wa gereza. 22 Kwa
hiyo msimamizi wa gereza akamweka
Yosefu awe mkuu wa wafungwa pamoja
na kusimamia yote ambayo yalitendeka
mle gerezani. 23 [d]Msimamizi wa gereza
hakujishughulisha tena na kitu chochote
kilichokuwa chini ya uangalizi wa Yosefu,
kwa sababu BWANA alikuwa pamoja na
Yosefu akimfanikisha kwa kila alichofanya.

### *Mnyweshaji Na Mwokaji*

40 Baada ya muda, mnyweshaji na
mwokaji wa mfalme wa Misri,
wakamkosea bwana wao, mfalme wa Misri.
2 [e]Farao akawakasirikia hawa maafisa wake
wawili, mnyweshaji mkuu na mwokaji
mkuu, 3 [f]akawaweka chini ya ulinzi katika
nyumba ya mkuu wa kikosi cha ulinzi
katika gereza lile lile alimofungwa Yosefu.
4 [g]Mkuu wa kikosi cha ulinzi akawakabidhi
kwa Yosefu, naye akawahudumia.
Walipokuwa wamekaa chini ya ulinzi
kwa muda, 5 kila mmoja wa hao wawili
waliokuwa wamewekwa gerezani, yaani
mnyweshaji na mwokaji wa mfalme wa
Misri, waliota ndoto usiku mmoja, na kila
ndoto ilikuwa na maana yake tofauti.
6 Yosefu alipowajia asubuhi yake,
akawaona kwamba walikuwa na huzuni.
7 Ndipo Yosefu akawauliza maafisa hao wa
Farao waliokuwa chini ya ulinzi pamoja
naye nyumbani mwa bwana wake, akasema,
“Mbona nyuso zenu zimejaa huzuni leo?”
8 [h]Wakamjibu, “Sisi sote tuliota ndoto,
lakini hapakuwa na mtu yeyote wa
kuzifasiri.”
Ndipo Yosefu akawaambia, “Je, kufasiri
ndoto si kazi ya Mungu? Niambieni ndoto
zenu.”
9 Basi mkuu wa wanyweshaji akamweleza
Yosefu ndoto yake. Akamwambia, “Katika
ndoto yangu niliona mzabibu mbele
yangu, 10 [i]nao mzabibu ulikuwa na matawi
matatu. Mara tu ulipoanza kuchipua, maua
yalichanua na vishada vyake vikawa zabibu
zilizoiva. 11 Kikombe cha Farao kilikuwa
mkononi mwangu, nikazitwaa zabibu,
nikazikamua katika kikombe cha Farao,
na nikaweka kikombe mkononi mwake.”
12 [j]Yosefu akamwambia, “Hii ndiyo
maana yake: Matawi matatu ni siku tatu.
13 [k]Katika siku hizi tatu, Farao atakutoa
gerezani na kukuweka tena kwenye nafasi
yako, nawe utaweka kikombe cha Farao
mikononi mwake, kama vile ulivyokuwa
unafanya ulipokuwa mnyweshaji wake.
14 [l]Lakini wakati mambo yatakapokuwia
mazuri, unikumbuke, unifanyie wema,
useme mema juu yangu kwa Farao ili
niondoke huku gerezani. 15 Kwa maana
nilichukuliwa kwa nguvu kutoka nchi ya
Waebrania, na hata hapa nilipo sikufanya
lolote linalostahili niwekwe gerezani.”
16 [m]Yule mwokaji mkuu alipoona kuwa
Yosefu amefasiri ikiwa na maana nzuri,
akamwambia Yosefu, “Mimi pia niliota
ndoto: Kichwani mwangu kulikuwepo

[a]**39:17** Kut 20:16; Mwa 14:13
[b]**39:20** Za 105:18
[c]**39:21** Kut 3:21; Mit 16:7
[d]**39:23** Mwa 21:20; Hes 14:43
[e]**40:2** Mit 16:14; Es 2:21
[f]**40:3** Mwa 37:36; 39:20
[g]**40:4** Mwa 37:36; 42:17
[h]**40:8** Mwa 41:8, 15; Kum 29:29
[i]**40:10** Isa 27:6; Hos 14:7
[j]**40:12** Dan 2:36
[k]**40:13** Yos 1:11
[l]**40:14** 1Sam 25:31; 1The 2:7
[m]**40:16** Amo 8:1-2

vikapu vitatu vya mikate. 17 Katika kikapu
cha juu kulikuwa na aina zote za vyakula
vilivyookwa kwa ajili ya Farao, lakini ndege
walikuwa wakivila kutoka kwenye kikapu
nilichokuwa nimebeba kichwani."

18 [a]Yosefu akamwambia, "Hii ndiyo
maana yake: Vikapu vitatu ni siku tatu.
19 [b]Katika siku hizi tatu, Farao atakata
kichwa chako na kukutundika juu ya mti.
Nao ndege watakula nyama ya mwili
wako."

20 Mnamo siku ya tatu, ilikuwa
kumbukumbu ya kuzaliwa kwa Farao,
naye akawaandalia maafisa wake wote
karamu. Akawatoa gerezani mnyweshaji
mkuu na mwokaji mkuu, akawaweka mbele
ya maafisa wake: 21 [c]Ndipo akamrudisha
mnyweshaji mkuu kwenye nafasi yake, ili
aweke kikombe mikononi mwa Farao tena,
22 lakini akamwangika yule mwokaji mkuu,
sawasawa na jinsi Yosefu alivyowaambia
katika tafsiri yake.

23 [d]Pamoja na hayo, mnyweshaji mkuu
hakumkumbuka Yosefu, bali alimsahau.

*Ndoto Za Farao*

41 [e]Baada ya miaka miwili kamili
kupita, Farao aliota ndoto: Tazama
alikuwa amesimama kando ya Mto Naili,
2 [f]wakati ng'ombe saba, wazuri na wanono,
walitokea mtoni wakajilisha kwenye
matete. 3 Baada yao ng'ombe wengine saba,
wabaya na waliokonda, wakatokea mtoni
Naili wakasimama kando ya wale wanono
ukingoni mwa mto. 4 [g]Wale ng'ombe
wabaya na waliokonda wakawala wale saba
wazuri na wanono. Kisha Farao akaamka.

5 Farao akaingia usingizini tena akaota
ndoto ya pili: Akaona masuke saba ya
nafaka, yenye afya na mazuri, yanakua
katika bua moja. 6 [h]Baadaye, masuke
mengine saba yakachipua, yakiwa
membamba yaliyonyaushwa na upepo
wa mashariki. 7 [i]Masuke yale membamba
yakameza yale masuke saba yenye afya
na yaliyojaa. Basi Farao akaamka kutoka
usingizini, kumbe ilikuwa ndoto.

8 [j]Asubuhi yake, alifadhaika akilini, hivyo
akawaita waaguzi wote pamoja na watu
wenye busara wa Misri. Walipokuja, Farao
akawaeleza ndoto zake, lakini hakuna hata
mmoja aliyeweza kumfasiria.

9 Ndipo mnyweshaji mkuu alipomwambia
Farao, "Leo nimekumbushwa kuhusu kosa
langu. 10 [k]Wakati fulani Farao aliwakasirikia
watumishi wake, akanifunga mimi na
mwokaji mkuu katika nyumba ya mkuu
wa ulinzi. 11 [l]Kila mmoja wetu aliota ndoto
katika usiku mmoja na kila ndoto ilikuwa
na maana yake tofauti. 12 [m]Basi kijana wa
Kiebrania aliyekuwa pamoja nasi huko,
alikuwa mtumishi wa mkuu wa kikosi
cha ulinzi. Tulimweleza ndoto zetu, naye
akatufasiria, akitupa kila mtu tafsiri ya
ndoto yake. 13 [n]Nayo mambo yakawa sawa
kabisa na jinsi alivyotufasiria ndoto zetu:
Mimi nilirudishwa kazini mwangu na huyo
mtu mwingine akaangikwa."

14 [o]Basi, Farao akatuma Yosefu aitwe,
naye akatolewa kifungoni haraka. Baada ya
kunyoa na kubadilisha nguo zake akaenda
mbele ya Farao.

15 [p]Farao akamwambia Yosefu, "Nimeota
ndoto, wala hakuna mtu hata mmoja
anayeweza kuifasiri. Lakini nimesikia
ikisemwa kwa habari yako kwamba
unapoelezwa ndoto waweza kuifasiri."

16 [q]Yosefu akamjibu Farao, "Siwezi
kuifasiri, lakini Mungu atampa Farao jibu
analolihitaji."

17 Kisha Farao akamwambia Yosefu,
"Katika ndoto yangu nilikuwa nimesimama
ukingoni mwa Mto Naili, 18 nikawaona

[a]**40:18** Mwa 40:12
[b]**40:19** Kum 21:22-23; 1Sam 17:44
[c]**40:21** 2Fal 25:27; Yer 52:31
[d]**40:23** Mhu 1:11
[e]**41:1** Kut 2:5
[f]**41:2** Ay 40:21
[g]**41:4** Mwa 41:7
[h]**41:6** Za 11:6
[i]**41:7** Mwa 41:4
[j]**41:8** Kut 7:11, 22; Dan 4:18
[k]**41:10** Mwa 40:2
[l]**41:11** Mwa 40:5
[m]**41:12** Mwa 40:12
[n]**41:13** Mwa 40:22
[o]**41:14** Za 105:20; Rut 3:3
[p]**41:15** Dan 5:16
[q]**41:16** Mwa 40:8

ng'ombe saba, wazuri na wanono,
wakijitokeza kutoka mtoni wakaja kujilisha
kwenye matete. 19 Baada ya hao, ng'ombe
wengine saba wadhaifu wakatokea, wabaya
sana na waliokonda. Kamwe sikuwahi kuona
ng'ombe wabaya jinsi hiyo katika nchi yote
ya Misri. 20 Hao ng'ombe waliokonda na
wabaya sana wakawala wale ng'ombe saba
walionona waliojitokeza kwanza. 21 Lakini
hata baada ya kuwala, hakuna mtu ambaye
angeweza kusema kwamba wamekula, bado
walionekana wabaya kama mwanzoni.
Kisha nikaamka kutoka usingizini.
22 "Pia katika ndoto zangu niliona masuke
saba ya nafaka, yamejaa na mazuri, yanakua
katika bua moja. 23 Baada ya hayo masuke
mengine saba yakachipua, yaliyonyauka,
membamba na yamekaushwa na upepo
wa mashariki. 24 Yale masuke membamba
ya nafaka yakayameza yale masuke saba
mazuri yaliyojaa nafaka. Nimewaeleza
waaguzi, wala hakuna yeyote aliyeweza
kunifasiria."
25 [a]Ndipo Yosefu akamwambia Farao,
"Ndoto za Farao ni ndoto iyo hiyo
moja. Mungu amemfunulia Farao jambo
analokusudia kufanya karibuni. 26 Ng'ombe
saba wazuri ni miaka saba, nayo masuke
saba mazuri yaliyojaa nafaka ni miaka saba,
ni ndoto iyo hiyo moja. 27 Ng'ombe saba
waliokonda na wabaya wale waliojitokeza
baadaye ni miaka saba, vivyo hivyo masuke
saba ya ngano yaliyodhoofika na kukaushwa
na upepo wa mashariki, ni miaka saba ya
njaa.
28 "Ni kama vile nilivyomwambia Farao:
Mungu amemwonyesha Farao jambo
analokusudia kufanya karibuni. 29 [b]Miaka
saba ya neema inakuja katika nchi yote ya
Misri, 30 [c]lakini itafuata miaka saba ya njaa.
Ndipo neema yote ya Misri itasahaulika na
njaa itaikumba nchi.
31 "Neema iliyokuwa katika nchi
haitakumbukwa, kwa sababu njaa
itakayofuata itakuwa kali mno. 32 Sababu
ya ndoto kumjia Farao kwa namna mbili ni
kwamba jambo hilo Mungu ameshaamua
kwa hakika, naye Mungu atalifanya
karibuni.
33 [d]"Basi sasa Farao na atafute mtu
mwenye akili na hekima ili amweke kuwa
msimamizi wa nchi ya Misri. 34 [e]Farao na
aweke wenye amri nchini kote wakusanye
sehemu ya tano ya mavuno ya Misri katika
miaka hii saba ya neema. 35 [f]Wakusanye
chakula chote katika miaka hii saba ya
neema inayokuja na kuhifadhi nafaka chini
ya mamlaka ya Farao, iwe akiba ya chakula
katika miji. 36 Chakula hiki kitakuwa akiba
ya tahadhari kwa ajili ya nchi, ili kitumike
katika ile miaka saba ya njaa itakayokuja
Misri, ili nchi isiharibiwe na njaa."
37 Mpango huu ulionekana mzuri kwa
Farao na kwa maafisa wake wote. 38 [g]Hivyo
Farao akawauliza, "Je tunaweza kumpata
yeyote kama mtu huyu, ambaye Roho wa
Mungu yumo ndani yake?"
39 Ndipo Farao akamwambia Yosefu,
"Maadamu Mungu amekufunulia yote haya,
hakuna mwingine yeyote mwenye akili na
hekima kama wewe. 40 [h]Wewe utakuwa
msimamizi wa jumba langu la kifalme, na
watu wangu wote watatii amri zako. Ni
kuhusu kiti cha ufalme tu nitakuwa mkuu
kuliko wewe."

*Yosefu Msimamizi Wa Misri*

41 [i]Kwa hiyo Farao akamwambia Yosefu,
"Sasa nakuweka uwe msimamizi wa nchi
yote ya Misri." 42 [j]Ndipo Farao akaivua pete
yake ya muhuri kutoka kidoleni mwake
na kuivalisha katika kidole cha Yosefu.
Akamvika majoho mazuri ya kitani safi
na mkufu wa dhahabu shingoni mwake.
43 [k]Akampandisha katika gari lake la farasi
kama msaidizi wake, watu wakatangulia
wakishangilia, wakisema, "Fungueni njia!"
Ndivyo Farao alivyomweka Yosefu kuwa
msimamizi wa nchi yote ya Misri.

[a]**41:25** Dan 2:45
[b]**41:29** Mwa 41:47
[c]**41:30** Mwa 41:54; 47:13
[d]**41:33** Mwa 41:39
[e]**41:34** Es 2:3
[f]**41:35** Mwa 41:48
[g]**41:38** Hes 27:18; Dan 4:8-9, 18; 5:11, 14
[h]**41:40** Za 105:21-22; Mdo 7:10
[i]**41:41** Mwa 42:6
[j]**41:42** Es 3:10; Dan 5:29
[k]**41:43** Isa 2:7

44 Kisha Farao akamwambia Yosefu,
"Mimi ni Farao, lakini pasipo neno lako,
hakuna mtu mwenye ruhusa kuinua
mkono au mguu katika nchi yote ya Misri."
45 [a]Farao akamwita Yosefu Safenath-Panea,
pia akampa Asenathi binti Potifera, kuhani
wa mji wa Oni,[b] kuwa mke wake. Ndipo
Yosefu akaitembelea nchi yote ya Misri.
46 [c]Yosefu alikuwa na miaka thelathini
alipoingia katika utumishi wa Farao mfalme
wa Misri. Naye Yosefu akatoka mbele ya
Farao akasafiri katika nchi yote ya Misri.
47 [d]Katika ile miaka saba ya neema nchi
ilizaa mazao kwa wingi sana. 48 [e]Yosefu
akakusanya chakula chote kilichozalishwa
katika ile miaka saba ya neema nchini Misri,
akakihifadhi katika ghala za miji. Katika kila
mji kulihifadhiwa chakula kilichozalishwa
katika mashamba yaliyouzunguka mji huo.
49 [f]Yosefu alihifadhi nafaka nyingi, mfano
wa mchanga wa bahari, ilikuwa nyingi
mno kiasi kwamba walishindwa kuweka
kumbukumbu kwa sababu akiba ilizidi sana
kupita kipimo.
50 Kabla ya miaka ya njaa kuanza,
Asenathi binti Potifera, kuhani wa mji
wa Oni, alikuwa amemzalia Yosefu wana
wawili wa kiume. 51 [g]Yosefu akamwita
mzaliwa wake wa kwanza Manase, akisema,
"Ni kwa sababu Mungu amenifanya nisahau
taabu zangu zote pamoja na jamaa yote
ya nyumba ya baba yangu." 52 [h]Mwana wa
pili akamwita Efraimu, akisema, "Ni kwa
sababu Mungu amenistawisha katika nchi
ya mateso yangu."
53 Ile miaka saba ya neema huko Misri
ikaisha, 54 [i]nayo miaka ile saba ya njaa
ikaanza, sawasawa na alivyosema Yosefu.
Kulikuwa na njaa katika nchi nyingine zote,
bali katika nchi yote ya Misri kulikuwa
na chakula. 55 Wakati nchi yote ya Misri
ilipopatwa na njaa, watu wakamlilia Farao
ili awape chakula. Ndipo Farao alipowaagiza
Wamisri wote, akisema, "Nendeni kwa
Yosefu, nanyi mfanye anachowaambia."
56 Wakati njaa ilipokuwa imeenea
katika nchi yote, Yosefu akafungua ghala
za vyakula na kuwauzia Wamisri nafaka,
kwa sababu njaa ilikuwa kali mno katika
nchi yote ya Misri. 57 Pia nchi nyingine zote
zilikuja Misri kununua nafaka kutoka kwa
Yosefu, kwa sababu njaa ilikuwa kali mno
duniani kote.

*Ndugu Za Yosefu Waenda Misri*

42 [j]Wakati Yakobo alipofahamu kuwa
kuna nafaka huko Misri, akawaambia
wanawe, "Mbona mnakaa tu hapa
mnatazamana?" 2 [k]Akaendelea kuwaambia,
"Nimesikia kuwa huko Misri kuna nafaka.
Telemkeni huko mkanunue chakula kwa
ajili yetu, ili tuweze kuishi wala tusife."
3 Ndipo wale ndugu kumi wa Yosefu,
wakateremka huko Misri kununua nafaka.
4 [l]Lakini Yakobo hakumtuma Benyamini,
ndugu yake Yosefu, pamoja na wengine,
kwa sababu aliogopa asije akapatwa
na madhara. 5 [m]Hivyo wana wa Israeli
walikuwa miongoni mwa wale waliokwenda
Misri kununua nafaka, kwani njaa ilikuwa
katika nchi ya Kanaani pia.
6 [n]Wakati huo Yosefu alikuwa mtawala wa
nchi ya Misri, naye alikuwa ndiye aliwauzia
watu wote nafaka. Kwa hiyo wakati ndugu
zake Yosefu walipofika, wakamsujudia hadi
nyuso zao zikagusa ardhi. 7 Mara Yosefu
alipowaona ndugu zake, akawatambua,
lakini akajifanya mgeni na kuzungumza
nao kwa ukali, akiwauliza, "Ninyi mnatoka
wapi?"

Wakamjibu, "Tumetoka katika nchi ya
Kanaani kuja kununua chakula."
8 Ingawa Yosefu aliwatambua ndugu
zake, wao hawakumtambua. 9 [o]Ndipo
Yosefu alipokumbuka ndoto zake kuwahusu

---

[a]**41:45** Es 2:7
[b]45 Yaani Heliopoli (Mji wa Jua).
[c]**41:46** Mit 22:29
[d]**41:47** Mwa 41:29
[e]**41:48** Mwa 41:34
[f]**41:49** Mwa 12:2
[g]**41:51** Hes 1:34
[h]**41:52** Mwa 17:6
[i]**41:54** Mdo 7:11
[j]**42:1** Mdo 7:12
[k]**42:2** Mwa 43:8
[l]**42:4** Mwa 42:38
[m]**42:5** Mdo 7:11
[n]**42:6** Mwa 41:41
[o]**42:9** Mwa 37:7

wao, akawaambia, “Ninyi ni wapelelezi!
Mmekuja kuangalia mahali ambapo nchi
yetu haina ulinzi.”
10 Wakamjibu, “Sivyo bwana wangu.
Watumishi wako wamekuja kununua
chakula. 11 Sisi sote ni wana wa baba mmoja.
Watumishi wako ni watu waaminifu, wala
sio wapelelezi.”
12 Akawaambia, “La hasha! Mmekuja
kuangalia mahali ambapo nchi yetu haina
ulinzi.”
13 [a]Lakini wakamjibu, “Watumishi wako
walikuwa kumi na wawili, wana wa mtu
mmoja ambaye anaishi katika nchi ya
Kanaani. Sasa mdogo wetu wa mwisho
yupo na baba yetu na mwingine alikufa.”
14 Yosefu akawaambia, “Ni sawa kabisa
kama nilivyowaambia: Ninyi ni wapelelezi!
15 [b]Na hivi ndivyo mtakavyojaribiwa:
Hakika kama Farao aishivyo, hamtaondoka
mahali hapa mpaka ndugu yenu mdogo aje
hapa. 16 [c]Tumeni mmoja wenu akamlete
huyo ndugu yenu, wengine mtawekwa
gerezani, ili maneno yenu yajaribiwe kuona
kama mnasema kweli. La sivyo, hakika
kama Farao aishivyo ninyi ni wapelelezi!”
17 [d]Akawaweka wote chini ya ulinzi kwa
siku tatu.
18 [e]Siku ya tatu Yosefu akawaambia,
“Fanyeni hili nanyi mtaishi, kwa maana
namwogopa Mungu: 19 Ikiwa ninyi ni watu
waaminifu, mmoja wa ndugu zenu na abaki
kifungoni, nanyi wengine pelekeni nafaka
kwa jamaa yenu wanaoteseka kwa njaa.
20 Lakini ni lazima mniletee ndugu yenu
mdogo hapa, ili maneno yenu yathibitike na
kwamba msife.” Wakakubali kufanya hivyo.
21 [f]Wakaambiana wao kwa wao, “Hakika
tunaadhibiwa kwa sababu ya ndugu yetu.
Tuliona jinsi alivyohuzunika alipokuwa
anatusihi kuponya maisha yake, lakini
hatukumsikiliza, hiyo ndiyo sababu dhiki
hii imetupata.”
22 [g]Reubeni akawajibu, “Sikuwaambieni
msitende dhambi dhidi ya kijana? Lakini
hamkunisikiliza! Sasa ni lazima tuadhibiwe
kwa ajili ya damu yake.” 23 [h]Hawakujua
kuwa Yosefu angewaelewa, kwa sababu
alitumia mkalimani.
24 [i]Yosefu akajitenga nao akaanza kulia,
kisha akawarudia na kuzungumza nao tena.
Akataka Simeoni akamatwe na kufungwa
mbele yao.
25 [j]Yosefu akatoa amri ya kujaza magunia
yao nafaka na kuweka fedha ya kila mmoja
ndani ya gunia lake, kisha wapewe mahitaji
ya njiani. Baada ya kufanyiwa hayo yote,
26 wakapakiza nafaka juu ya punda zao,
wakaondoka.
27 [k]Walipofika mahali pa kulala huko
njiani mmoja wao akafungua gunia lake
ili amlishe punda wake, akakuta fedha
yake kwenye mdomo wa gunia lake.
28 [l]Akawaambia ndugu zake, “Fedha yangu
imerudishwa. Iko ndani ya gunia langu.”
Mioyo yao ikazimia, na kila mmoja
akamgeukia mwenzake wakitetemeka,
wakaulizana, “Ni nini hiki Mungu
alichotufanyia?”
29 [m]Walipofika kwa Yakobo baba yao
katika nchi ya Kanaani, wakamweleza
mambo yote yaliyowapata. Wakasema,
30 [n]“Huyo mtu ambaye ndiye bwana
katika nchi hiyo alisema nasi kwa ukali,
akatutendea kana kwamba sisi tulikuwa
tunaipeleleza nchi. 31 Lakini tulimwambia,
‘Sisi ni watu waaminifu, sio wapelelezi.
32 Tulizaliwa ndugu kumi na wawili, wana
wa baba mmoja. Mmoja alikufa, na mdogo
wetu wa mwisho yupo na baba yetu huko
Kanaani.’
33 “Ndipo huyo mtu aliye bwana katika
nchi hiyo alipotuambia, ‘Hivi ndivyo
nitafahamu kuwa ninyi ni watu waaminifu:
Mwacheni mmoja wa ndugu zenu pamoja

[a]**42:13** Mwa 37:33
[b]**42:15** 1Sam 17:55
[c]**42:16** Mwa 42:11
[d]**42:17** Mwa 40:4
[e]**42:18** Law 25:43
[f]**42:21** Mwa 45:5
[g]**42:22** Mwa 9:5
[h]**42:23** Mwa 11:7
[i]**42:24** Mwa 43:14, 23
[j]**42:25** Yer 40:5
[k]**42:27** Isa 1:3
[l]**42:28** Mk 5:3
[m]**42:29** Mwa 44:24
[n]**42:30** Mwa 42:7

nami hapa, kisha nendeni mpeleke chakula
kwa ajili ya jamaa yenu inayoteseka kwa
njaa. 34 [a]Lakini mleteni huyo ndugu yenu
mdogo kwangu, ndipo nitajua kuwa ninyi
sio wapelelezi, ila ni watu waaminifu. Kisha
nitamrudisha ndugu yenu, nanyi mtaweza
kufanya biashara katika nchi hii.' "

35 Walipokuwa wanamimina nafaka
kutoka kwenye magunia yao, ndani ya gunia
la kila mtu kulikuwa na mfuko wa fedha!
Wakati wao na baba yao walipoona mifuko
ya fedha, wakaogopa. 36 [b]Yakobo baba
yao akawaambia, "Ninyi mmenipokonya
watoto wangu. Yosefu hayupo na Simeoni
hayupo tena na sasa mnataka kumchukua
Benyamini. Kila kitu ni kinyume nami!"

37 Ndipo Reubeni akamwambia baba
yake, "Waweza kuwaua wanangu wote
wawili, ikiwa sitamrudisha Benyamini
kwako. Mkabidhi Benyamini katika
uangalizi wangu, nami nitamrudisha."

38 [c]Lakini Yakobo akasema, "Mwanangu
hatashuka huko pamoja nanyi; ndugu yake
amekufa naye ndiye peke yake aliyebaki.
Ikiwa atapatwa na madhara katika safari
mnayoiendea, mtashusha kichwa changu
chenye mvi kaburini kwa masikitiko."

### *Safari Ya Pili Ya Kwenda Misri*

43 [d]Wakati huu njaa ilikuwa bado ni
kali mno katika nchi. 2 Hivyo wakati
walikuwa wamemaliza kula nafaka yote
waliyoileta kutoka Misri, Yakobo baba yao
akawaambia, "Rudini Misri mkatununulie
chakula kingine zaidi."

3 [e]Lakini Yuda akamwambia, "Mtu yule
alituonya kwa msisitizo, 'Hamtauona uso
wangu tena mpaka mje na ndugu yenu.'
4 Kama utakubali ndugu yetu aende
pamoja nasi, tutakwenda kuwanunulia
chakula. 5 [f]Lakini ikiwa hutamruhusu
aende, hatutakwenda, kwa sababu mtu
yule alituambia, 'Hamtauona uso wangu
tena mpaka mje pamoja na ndugu yenu.' "

6 [g]Israeli akauliza, "Kwa nini mkaniletea
taabu hii kwa kumwambia yule mtu
mlikuwa na ndugu mwingine?"

7 [h]Wakamjibu, "Yule mtu alituhoji kwa
undani sana habari zetu na za jamaa yetu.
Alituuliza, 'Je, baba yenu bado yungali
hai? Je mnaye ndugu mwingine?' Sisi
tulimjibu maswali yake tu. Tungewezaje
kujua kwamba angesema, 'Mleteni mdogo
wenu hapa'?"

8 Ndipo Yuda akamwambia baba
yake Israeli, "Mtume kijana pamoja
nami, nasi tutaondoka mara, ili sisi na
wewe pamoja na watoto wetu tuweze
kuishi, wala tusife. 9 [i]Mimi mwenyewe
nitakuhakikishia usalama wake, mimi
mwenyewe nitawajibika kumrudisha. Ikiwa
sitamrudisha kwako na kumweka mbele
yako, nitakuwa mwenye lawama mbele
yako maisha yangu yote. 10 [j]Hakika, kama
hatukuchelewa kuondoka, tungekuwa
tumekwenda na kurudi mara mbili."

11 [k]Basi baba yao Israeli akawaambia,
"Kama ni lazima iwe hivyo, basi fanyeni
hivi: Wekeni baadhi ya mazao bora ya
nchi katika mifuko yenu na mpelekeeni
yule mtu kama zawadi, zeri kidogo, asali
kidogo, vikolezo, manemane, kungu na
lozi. 12 [l]Chukueni fedha mara mbili, kwa
kuwa mtazirudisha zile fedha zilizowekwa
midomoni mwa magunia yenu. Labda
ziliwekwa kwa makosa. 13 Mchukueni
ndugu yenu pia mrudi kwa huyo mtu
mara moja. 14 [m]Naye Mungu Mwenyezi[n]
awajalieni rehema mbele ya huyo mtu
ili apate kumwachia yule ndugu yenu na
Benyamini mweze kurudi pamoja. Kwangu
mimi kama nikufiwa nimefiwa."

15 Basi hao watu wakazichukua zile
zawadi na zile fedha mara mbili pamoja

---

[a]**42:34** Mwa 34:10
[b]**42:36** Mwa 42:24
[c]**42:38** Mwa 37:33
[d]**43:1** Mwa 12:10
[e]**43:3** Mwa 42:15
[f]**43:5** 2Sam 3:13
[g]**43:6** Mwa 34:30
[h]**43:7** Mwa 42:13
[i]**43:9** Mwa 42:37; Flm 18-19
[j]**43:10** Mwa 45:9
[k]**43:11** Mwa 37:25
[l]**43:12** Mwa 42:25
[m]**43:14** Kum 13:17
[n]14 Mungu Mwenyezi hapa ni jina la Kiebrania, El-Shaddai (yaani Mungu Mwenye utoshelevu wote).

na Benyamini. Wakafanya haraka kwenda
Misri na walipofika wakajionyesha kwa
Yosefu. 16 [a]Yosefu alipomwona Benyamini
pamoja nao, akamwambia msimamizi wa
nyumba yake, "Wachukue watu hawa
nyumbani kwangu, mchinje mnyama na
kuandalia chakula kwa kuwa watakula
chakula cha mchana pamoja nami."
17 [b]Yule Msimamizi akafanya kama Yosefu
alivyomwambia na akawachukua wale
watu nyumbani kwa Yosefu. 18 [c]Basi watu
hao wakaogopa walipopelekwa nyumbani
kwa Yosefu. Wakafikiri, "Tumeletwa hapa
kwa ajili ya zile fedha zilizorudishwa katika
magunia yetu mara ile ya kwanza. Anataka
kutushambulia na kutushinda, atuchukue
sisi kama watumwa, na atwae hawa punda
zetu."
19 Hivyo wakamwendea msimamizi wa
nyumba wa Yosefu na kuzungumza naye
kwenye ingilio la nyumbani. 20 [d]Wakasema,
"Tafadhali bwana, tulikuja hapa mara ya
kwanza kununua chakula. 21 [e]Lakini mahali
pale tulipotua wakati wa jioni tulifungua
magunia yetu, na kila mmoja wetu
akakuta fedha zake, kwenye mdomo wa
gunia lake kiasi kile kile tulicholeta. Kwa
hiyo tumezirudisha. 22 Pia tumeleta fedha
nyingine kwa ajili ya kununulia chakula.
Hatujui ni nani aliziweka fedha hizo katika
magunia yetu."
23 Akawaambia, "Vema, msiogope.
Mungu wenu, Mungu wa baba yenu,
amewapa ninyi hazina katika magunia
yenu; mimi nilipokea fedha yenu." Ndipo
akawaletea Simeoni.
24 [f]Msimamizi akawapeleka wale watu
katika nyumba ya Yosefu, akawapa maji
ya kunawa miguu na kuwapa punda
wao majani. 25 [g]Wakaandaa zawadi zao
ili wampe Yosefu wakati atakapofika
adhuhuri, kwa kuwa walikuwa wamesikia
kwamba watakula chakula huko.
26 [h]Yosefu alipokuja nyumbani,
walimkabidhi zile zawadi walizokuwa
nazo, ambazo walikuwa wamezileta mle
nyumbani, nao wakamsujudia hadi nchi.
27 [i]Akawauliza kuhusu hali yao, kisha
akawaambia, "Yule baba yenu mzee
mliyeniambia habari zake, yu hali gani?
Je, bado yu hai?"
28 [j]Wakamjibu, "Mtumishi wako baba
yetu bado anaishi na ni mzima." Kisha
wakainama chini kumpa heshima.
29 [k]Alipotazama na kumwona Benyamini
ndugu yake, mwana wa mama yake hasa,
akauliza, "Je, huyu ndiye ndugu yenu wa
mwisho, ambaye mlinieleza habari zake?"
Ndipo akasema, "Mungu na akufadhili,
mwanangu." 30 Akiwa ameguswa sana kwa
kumwona ndugu yake, Yosefu akatoka nje
kwa haraka na kutafuta mahali pa kulilia.
Akaingia kwenye chumba chake cha pekee
na kulilia humo.
31 Baada ya kunawa uso wake, akatoka
nje na huku akijizuia akasema, "Pakueni
chakula."
32 [l]Wakampakulia Yosefu peke yake,
ndugu zake peke yao na Wamisri waliokula
pamoja naye peke yao, kwa sababu Wamisri
wasingeweza kula pamoja na Waebrania,
kwa maana ilikuwa ni chukizo kwa
Wamisri. 33 Watu hao walikuwa wameketi
mbele yake kwa mfuatano wa umri wao,
kuanzia mzaliwa wa kwanza hadi mzaliwa
wa mwisho, wakatazamana wao kwa wao
kwa mshangao. 34 [m]Wakati walipelekewa
sehemu ya chakula kutoka mezani mwa
Yosefu, sehemu ya Benyamini ilikuwa mara
tano zaidi ya sehemu ya wale wengine. Kwa
hiyo wakanywa na kufurahi pamoja naye.

### *Kikombe Cha Fedha Ndani Ya Gunia*

44 Kisha Yosefu akampa yule msimamizi
wa nyumbani mwake maagizo haya:
"Jaza magunia ya watu hawa kiasi cha
chakula ambacho wanaweza kuchukua, na

[a]**43:16** Mwa 44:1, 4, 12
[b]**43:17** Mwa 43:16
[c]**43:18** Mwa 44:14
[d]**43:20** Mwa 42:3
[e]**43:21** Mwa 43:15
[f]**43:24** Mwa 43:16; 18:4
[g]**43:25** Mwa 32:13
[h]**43:26** Mt 2:11
[i]**43:27** Mwa 37:3
[j]**43:28** Mwa 37:7
[k]**43:29** Mwa 42:13
[l]**43:32** Mwa 46:34
[m]**43:34** Mwa 37:3

uweke fedha ya kila mtu kwenye mdomo wa
gunia lake. 2 [a]Kisha weka kikombe changu
kile cha fedha kwenye mdomo wa gunia la
yule mdogo wa wote pamoja na fedha zake
ambazo angenunulia nafaka yake.” Naye
akafanya kama Yosefu alivyosema.
3 [b]Kulipopambazuka, hao watu
wakaruhusiwa kuondoka pamoja na punda
zao. 4 Kabla hawajafika mbali kutoka
mjini, Yosefu akamwambia mtumishi
wake, “Wafuatilie wale watu mara moja,
utakapowakuta, waambie, ‘Kwa nini
mmelipiza wema kwa ubaya? 5 [c]Je, kikombe
hiki sicho anachonywea bwana wangu na
pia hukitumia kwa kutabiri mambo yajayo?
Hili ni jambo ovu mlilolitenda.’ ”
6 Alipowafikia, akarudia maneno haya
kwao. 7 [d]Lakini wakamwambia mtumishi,
“Kwa nini bwana wangu anasema maneno
kama haya? Liwe mbali na watumishi wako
wasije wakafanya jambo kama hilo! 8 [e]Hata
hivyo tulikurudishia zile fedha kutoka nchi
ya Kanaani ambazo tulizikuta kwenye
midomo ya magunia yetu. Hivyo kwa nini
tuibe fedha au dhahabu kutoka nyumbani
kwa bwana wako? 9 [f]Ikiwa yeyote miongoni
mwa watumishi wako atapatikana nacho,
auawe, na sisi wengine tutakuwa watumwa
wa bwana wangu.”
10 Akajibu, “Vema sana; na iwe kama
msemavyo. Yeyote atakayekutwa nacho
atakuwa mtumwa wangu, lakini ninyi
wengine mtakuwa hamna lawama.”
11 Kila mmoja wao akafanya haraka
kushusha gunia lake chini na kulifungua.
12 Ndipo msimamizi akaendelea kutafuta,
akianzia kwa mkubwa wa wote na akaishia
kwa mdogo wa wote. Basi kikombe
kikapatikana katika gunia la Benyamini.
13 [g]Kwa jambo hili, wakararua nguo zao.
Ndipo wote wakapakiza mizigo yao juu ya
punda zao na kurudi mjini.
14 [h]Yosefu alikuwa bado yuko nyumbani
mwake wakati Yuda na kaka zake
walipoingia, wote wakajitupa chini mbele
yake. 15 [i]Yosefu akawaambia, “Ni jambo
gani hili mlilolifanya? Hamjui kuwa mtu
kama mimi anaweza kufahamu mambo kwa
njia ya kutabiri?”
16 [j]Yuda akajibu, “Tutaweza kusema nini
kwa bwana wangu? Tutaweza kuzungumza
nini? Tutawezaje kuthibitisha kwamba
hatuna hatia? Mungu amefunua hatia ya
watumishi wako. Sasa sisi tu watumwa wa
bwana wangu, sisi wenyewe pamoja na yule
aliyepatikana na kikombe.”
17 Lakini Yosefu alisema, “Liwe mbali
nami kufanya jambo kama hili! Mtu yule tu
aliyekutwa na kikombe ndiye atakayekuwa
mtumwa wangu. Ninyi wengine, rudini kwa
baba yenu kwa amani.”
18 [k]Ndipo Yuda akamwendea na
kumwambia: “Tafadhali bwana wangu,
mruhusu mtumishi wako aseme neno kwa
bwana wangu. Usimkasirikie mtumishi
wako, ingawa wewe ni sawa na Farao
mwenyewe. 19 Bwana wangu aliwauliza
watumishi wake, ‘Mnaye baba au ndugu?’
20 [l]Nasi tukakujibu, ‘Tunaye baba yetu
ambaye ni mzee; pia yupo mwanawe mdogo
aliyezaliwa katika uzee wake. Ndugu yake
amekufa, na huyu mdogo ndiye mwana
pekee kwa mama yake aliyebaki, naye baba
yake ampenda.’
21 [m]“Ndipo ulipowaambia watumishi
wako, ‘Mleteni kwangu ili niweze kumwona
kwa macho yangu mwenyewe.’ 22 Nasi
tukamwambia bwana wangu, ‘Kijana
hawezi kumwacha baba yake; akimwacha,
baba yake atakufa.’ 23 [n]Lakini ukawaambia
watumishi wako, ‘Ndugu yenu mdogo
asiposhuka pamoja nanyi, hamtauona uso
wangu tena.’ 24 [o]Tuliporudi nyumbani kwa

[a]**44:2** Mwa 44:8
[b]**44:3** Amu 19:9
[c]**44:5** Mwa 30:27
[d]**44:7** Mwa 18:5
[e]**44:8** Mwa 42:25
[f]**44:9** Mwa 31:32
[g]**44:13** Mwa 37:29
[h]**44:14** Mwa 33:3
[i]**44:15** Za 26:6
[j]**44:16** Mwa 37:8; Za 26:6
[k]**44:18** Mwa 18:30
[l]**44:20** Mwa 37:3; 42:13
[m]**44:21** Mwa 42:15
[n]**44:23** Mwa 43:5
[o]**44:24** Mwa 43:28

mtumwa wako baba yangu, tulimwambia
lile bwana wangu alilokuwa amesema.
25 [a]“Ndipo baba yetu aliposema, ‘Rudini
Misri mkanunue chakula kingine.’ 26 [b]Lakini
tukamwambia, ‘Hatuwezi kushuka Misri
mpaka ndugu yetu mdogo awe pamoja
nasi ndipo tutakapokwenda. Hatutaweza
kuuona uso wa yule mtu mpaka ndugu yetu
mdogo awe pamoja nasi.’
27 [c]“Mtumwa wako baba yangu
alituambia, ‘Mnajua mke wangu alinizalia
wana wawili. 28 [d]Mmojawapo alipotea,
nami nikasema, “Hakika ameraruliwa
vipande vipande.” Nami sijamwona tangu
wakati huo. 29 [e]Ikiwa mtaniondolea huyu
tena na akapatwa na madhara, mtashusha
kichwa changu chenye mvi kaburini nikiwa
mwenye huzuni.’
30 [f]“Hivyo sasa, kama kijana hatakuwa
pamoja nasi nitakaporudi kwa mtumishi
wako baba yangu, na kama baba yangu,
ambaye maisha yake yamefungamanishwa
na uhai wa kijana huyu, 31 akiona kijana
hayupo nasi, atakufa. Watumishi wako
watashusha kichwa chenye mvi cha baba
yetu kaburini kwa huzuni. 32 Mtumwa wako
alimhakikishia baba yangu usalama wa
kijana. Nikamwambia, ‘Kama sikumrudisha
kwako nitakuwa mwenye lawama mbele
yako, baba yangu, maisha yangu yote!’
33 “Sasa basi, tafadhali mruhusu mtumishi
abaki hapa kama mtumwa wa bwana wangu
badala ya kijana, naye kijana umruhusu
arudi na ndugu zake. 34 Ninawezaje kurudi
kwa baba yangu kama kijana hatakuwa
pamoja nami? La hasha! Usiniache nikaone
huzuni ile itakayompata baba yangu.”

*Yosefu Anajitambulisha*

45 [g]Hapo Yosefu hakuweza kujizuia
zaidi mbele ya wote waliokuwa
wamesimama karibu naye, akapaza sauti,
akasema, “Mwondoeni kila mtu mbele
yangu!” Kwa hiyo hapakuwepo mtu yeyote
pamoja na Yosefu alipojitambulisha kwa
ndugu zake. 2 [h]Naye akalia kwa sauti kubwa
kiasi kwamba Wamisri walimsikia, hata
watu wa nyumbani mwa Farao wakapata
hizo habari.
3 [i]Yosefu akawaambia ndugu zake, “Mimi
ni Yosefu! Je, baba yangu angali hai bado?”
Lakini ndugu zake hawakuweza kumjibu,
kwa sababu walipatwa na hofu kuu mbele
yake.
4 [j]Ndipo Yosefu akawaambia ndugu
zake, “Sogeeni karibu nami.” Waliposogea,
akasema, “Mimi ni ndugu yenu Yosefu,
yule ambaye mlimuuza Misri! 5 [k]Sasa,
msihuzunike wala msijichukie wenyewe
kwa kuniuza huku, kwa sababu ilikuwa ni
ili kuokoa maisha ya watu ndiyo sababu
Mungu alinituma niwatangulie ninyi.
6 Kwa miaka miwili sasa imekuwepo
njaa katika nchi, pia kwa miaka mitano
ijayo hapatakuwepo kulima wala kuvuna.
7 Lakini Mungu alinitanguliza mbele yenu
ili kuhifadhi mabaki kwa ajili yenu katika
nchi, na kuokoa maisha yenu kwa wokovu
mkuu.
8 [l]“Kwa hiyo basi, si ninyi mlionileta
huku, bali ni Mungu. Alinifanya kuwa baba
kwa Farao, bwana wa watu wa nyumbani
mwake wote, na mtawala wa Misri yote.
9 Sasa rudini haraka kwa baba yangu na
mwambieni, ‘Hili ndilo mwanao Yosefu
asemalo: Mungu amenifanya mimi kuwa
bwana wa Misri yote. Shuka uje kwangu,
wala usikawie. 10 [m]Nawe utaishi katika nchi
ya Gosheni na kuwa karibu nami, wewe,
watoto wako na wajukuu wako, makundi
yako ya kondoo, mbuzi na ng’ombe, pamoja
na vyote ulivyo navyo. 11 Nitawatunza
huko, kwa sababu bado iko miaka mingine
mitano inayokuja ya njaa. La sivyo, wewe
na nyumba yako na wote ulio nao mtakuwa
fukara.’
12 “Mnaweza kujionea wenyewe,

[a]**44:25** Mwa 42:2
[b]**44:26** Mwa 43:5
[c]**44:27** Mwa 46:19
[d]**44:28** Mwa 37:33
[e]**44:29** Mwa 42:38
[f]**44:30** 1Sam 18:1
[g]**45:1** 2Sam 13:9
[h]**45:2** Mdo 7:13
[i]**45:3** Mwa 43:7
[j]**45:4** Mwa 37:28
[k]**45:5** Mwa 50:20; Za 105:17
[l]**45:8** Amu 17:10; Mwa 41:41
[m]**45:10** Mwa 47:1

hata ndugu yangu Benyamini, kwamba
hakika ni mimi ninayezungumza nanyi.
13 [a]Mwambieni baba yangu juu ya heshima
yote niliyopewa huku Misri, na kuhusu kila
kitu mlichokiona. Mleteni baba yangu huku
haraka."

14 [b]Ndipo akamkumbatia Benyamini
ndugu yake na kulia, naye Benyamini
akamkumbatia akilia. 15 [c]Pia akawabusu
ndugu zake wote, huku akilia. Baada ya
hayo ndugu zake wakazungumza naye.

16 [d]Habari zilipofika kwenye jumba
la Farao kwamba ndugu zake Yosefu
wamefika, Farao na maafisa wake wote
wakafurahi. 17 [e]Farao akamwambia Yosefu,
"Waambie ndugu zako, 'Fanyeni hivi:
Pakieni wanyama wenu mrudi mpaka
nchi ya Kanaani, 18 [f]mkamlete baba yenu
na jamaa zenu kwangu. Nitawapa sehemu
nzuri sana ya nchi ya Misri nanyi mtafurahia
unono wa nchi.'

19 [g]"Mnaagizwa pia kuwaambia, 'Fanyeni
hivi: Chukueni magari ya kukokotwa
kutoka Misri, kwa ajili ya watoto wenu
na wake zenu, mkamchukue baba yenu
mje. 20 Msijali kamwe kuhusu mali zenu,
kwa sababu mema yote ya Misri yatakuwa
yenu.' "

21 Hivyo wana wa Israeli wakafanya
hivyo. Yosefu akawapa magari ya
kukokotwa, kama Farao alivyoagiza,
pia akawapa mahitaji kwa ajili ya safari
yao. 22 Kila mmoja mavazi mapya, lakini
Benyamini akampa shekeli 300[h] za fedha,
na jozi tano za nguo. 23 Hivi ndivyo vitu
alivyotuma kwa baba yake: punda kumi
waliochukua vitu vizuri vya Misri, punda
wake kumi waliobeba nafaka, mikate na
mahitaji mengine ya safari. 24 Akaagana
na ndugu zake walipokuwa wakiondoka,
akawaambia, "Msigombane njiani!"

25 Basi wakatoka Misri na kufika kwa
baba yao Yakobo katika nchi ya Kanaani.
26 Wakamwambia baba yao, "Yosefu
angali hai! Ukweli ni kwamba yeye ndiye
mtawala wa Misri yote." Yakobo akapigwa
na bumbuazi; hakuwasadiki. 27 [i]Lakini
walipokwisha kumweleza kila kitu ambacho
Yosefu alikuwa amewaambia, na alipoona
magari ya kukokotwa Yosefu aliyokuwa
amempelekea ya kumchukua aende Misri,
roho ya baba yao Yakobo ikahuishwa.
28 Ndipo Israeli akasema, "Nimesadiki!
Mwanangu Yosefu bado yu hai. Nitakwenda
nikamwone kabla sijafa."

### *Yakobo Aenda Misri*

46 Hivyo Israeli akaondoka na vyote
vilivyokuwa mali yake, naye alipofika
Beer-Sheba, akamtolea dhabihu Mungu wa
Isaki baba yake.

2 [j]Mungu akanena na Israeli katika maono
usiku na kusema, "Yakobo! Yakobo!"

Akajibu, "Mimi hapa."

3 [k]Mungu akamwambia, "Mimi ndimi
Mungu wa baba yako, usiogope kushuka
Misri, kwa maana huko nitakufanya taifa
kubwa. 4 [l]Nitashuka Misri pamoja nawe,
nami hakika nitakurudisha tena Kanaani.
Mikono ya Yosefu mwenyewe ndiyo
itakayofunga macho yako."

5 [m]Ndipo Yakobo akaondoka Beer-Sheba
nao wana wa Israeli wakamchukua baba
yao Yakobo na watoto wao na wake zao
katika magari ya kukokotwa yale Farao
aliyokuwa amempelekea kumsafirisha.
6 [n]Wakachukua pia mifugo yao na mali
walizokuwa wamezipata Kanaani, Yakobo
na uzao wake wote wakashuka Misri.
7 Akawachukua wanawe na binti zake,
wajukuu wake wa kiume na wa kike, yaani
uzao wake wote mpaka Misri.

8 Haya ndiyo majina ya wana wa Israeli
(Yakobo na wazao wake), waliokwenda
Misri:

---

[a]**45:13** Mdo 7:14
[b]**45:14** Mwa 29:13
[c]**45:15** Lk 15:20
[d]**45:16** Mwa 41:37
[e]**45:17** Mwa 42:5
[f]**45:18** Mwa 46:34; 47:6, 11, 27
[g]**45:19** Mwa 46:5
[h]22 Shekeli 300 za fedha ni sawa na kilo 3.4.

[i]**45:27** Mwa 45:19
[j]**46:2** Mwa 15:1
[k]**46:3** Mwa 12:2; 28:13
[l]**46:4** Mwa 5:16
[m]**46:5** Mwa 45:19
[n]**46:6** Kum 26:5; Mdo 7:15

Reubeni mzaliwa wa kwanza wa
Yakobo.
9 Wana wa Reubeni ni:
Hanoki, Palu, Hesroni na Karmi.
10 [a]Wana wa Simeoni ni:
Yemueli, Yamini, Ohadi, Yakini,
Sohari na Shauli mwana wa
mwanamke Mkanaani.
11 Wana wa Lawi ni:
Gershoni, Kohathi na Merari.
12 [b]Wana wa Yuda ni:
Eri, Onani, Shela, Peresi na Zera
(lakini Eri na Onani walifariki
katika nchi ya Kanaani).
Wana wa Peresi ni:
Hesroni na Hamuli.
13 Wana wa Isakari ni:
Tola, Puva, Yashubu na Shimroni.
14 [c]Wana wa Zabuloni ni:
Seredi, Eloni na Yaleeli.

15 [d]Hawa ndio wana wa Lea aliomzalia Yakobo huko Padan-Aramu pamoja na binti yake Dina. Jumla ya wanawe na binti zake walikuwa thelathini na watatu.

16 [e]Wana wa Gadi ni:
Sefoni, Hagi, Shuni, Esboni, Eri,
Arodi na Areli.
17 [f]Wana wa Asheri ni:
Imna, Ishva, Ishvi na Beria.
Dada yao alikuwa Sera.
Wana wa Beria ni:
Heberi na Malkieli.

18 Hawa ndio watoto Zilpa aliomzalia Yakobo, ambao Labani alimpa binti yake Lea; jumla yao walikuwa kumi na sita.

19 Wana wa Raheli mke wa Yakobo ni:
Yosefu na Benyamini.
20 [g]Huko
Misri, Asenathi binti wa Potifera,
aliyekuwa kuhani wa mji wa Oni,[h]
alimzalia Yosefu wana wawili,
Manase na Efraimu.
21 [i]Wana wa Benyamini ni:
Bela, Bekeri, Ashbeli, Gera,
Naamani, Ehi, Roshi, Mupimu,
Hupimu na Ardi.

22 Hawa ndio wana wa Raheli aliomzalia Yakobo; jumla yao ni kumi na wanne.

23 Mwana wa Dani ni:
Hushimu.
24 [j]Wana wa Naftali ni:
Yaseeli, Guni, Yeseri na Shilemu.

25 [k]Hawa walikuwa wana wa Bilha aliomzalia Yakobo, ambaye Labani alikuwa amempa Raheli binti yake; jumla yao walikuwa saba.

26 [l]Wote waliokwenda Misri pamoja na
Yakobo, waliokuwa wazao wake hasa pasipo
kuhesabu wakwe zake, walikuwa watu
sitini na sita.
27 [m]Pamoja na wana wawili
waliozaliwa na Yosefu huko Misri, jumla
yote ya jamaa ya Yakobo, waliokwenda
Misri, walikuwa sabini.

28 [n]Basi Yakobo akamtanguliza Yuda
aende kwa Yosefu ili amwelekeze njia
ya Gosheni. Walipofika nchi ya Gosheni,
29 [o]gari kubwa zuri la Yosefu liliandaliwa,
naye akaenda Gosheni kumlaki baba yake
Israeli. Mara Yosefu alipofika mbele yake,
alimkumbatia baba yake, akalia kwa muda
mrefu.
30 [p]Israeli akamwambia Yosefu, "Sasa niko tayari kufa, kwa kuwa nimejionea mwenyewe kwamba bado uko hai."
31 [q]Ndipo Yosefu akawaambia ndugu zake na watu wa nyumbani mwa baba yake, "Nitapanda kwa Farao na kumwambia, 'Ndugu zangu na watu wa nyumbani mwa baba yangu, waliokuwa wakiishi katika nchi

[a]**46:10** Kut 6:15
[b]**46:12** 1Nya 2:5; Mt 1:3
[c]**46:14** Mwa 30:20
[d]**46:15** Mwa 30:21
[e]**46:16** Hes 26:15
[f]**46:17** Mwa 30:13
[g]**46:20** Mwa 41:51
[h]20 Yaani Heliopoli (Mji wa Jua).
[i]**46:21** 1Nya 7:6-12
[j]**46:24** Mwa 30:8
[k]**46:25** Mwa 30:8
[l]**46:26** Kut 1:5; Kum 10:22
[m]**46:27** Mdo 7:14
[n]**46:28** Mwa 45:10
[o]**46:29** Mwa 29:11
[p]**46:30** Mwa 44:28
[q]**46:31** Mwa 45:10

ya Kanaani, wamekuja kwangu. 32 [a]Watu hao ni wachunga mifugo, huchunga mifugo, wamekuja na makundi ya kondoo, mbuzi na ng'ombe pamoja na kila kitu walicho nacho.' 33 [b]Farao atakapowaita na kuwaulizeni, 'Kazi yenu ni nini?' 34 [c]Mjibuni, 'Watumwa wako wamekuwa wachunga mifugo tangu ujana wetu mpaka sasa, kama baba zetu walivyofanya.' Ndipo mtakaporuhusiwa kukaa katika nchi ya Gosheni, kwa kuwa wachunga mifugo wote ni chukizo kwa Wamisri."

### *Yakobo Ambariki Farao*

47 [d]Yosefu akaenda na kumwambia Farao, "Baba yangu na ndugu zangu wamekuja kutoka nchi ya Kanaani wakiwa na makundi yao ya kondoo, mbuzi na ng'ombe, pamoja na kila kitu walicho nacho, nao sasa wapo huko Gosheni." 2 Akachagua ndugu zake watano na kuwaonyesha kwa Farao.

3 [e]Farao akawauliza hao ndugu zake, "Kazi yenu ni nini?"

Wakamjibu, "Watumishi wako ni wachunga mifugo, kama vile baba zetu walivyokuwa." 4 [f]Pia wakamwambia Farao, "Tumekuja kukaa huku kwa muda mfupi, kwa sababu njaa ni kali huko Kanaani, na mifugo ya watumishi wako haina malisho. Kwa hiyo sasa, tafadhali uruhusu watumishi wako wakae huko Gosheni."

5 Farao akamwambia Yosefu, "Baba yako na ndugu zako wamekuja kwako, 6 [g]nayo nchi ya Misri ipo mbele yako, uwakalishe baba yako na ndugu zako katika sehemu iliyo bora kupita zote katika nchi. Na waishi Gosheni. Kama unamfahamu yeyote miongoni mwao mwenye uwezo maalum, waweke wawe wasimamizi wa mifugo yangu."

7 [h]Ndipo Yosefu akamleta Yakobo baba yake na kumtambulisha mbele ya Farao. Baada ya Yakobo kumbariki Farao, 8 Farao akamuuliza, "Je una umri gani?"

9 [i]Naye Yakobo akamwambia Farao, "Siku za miaka ya kusafiri kwangu ni miaka 130. Miaka yangu imekuwa michache na ya taabu, wala haikufikia miaka ya kusafiri ya baba zangu." 10 [j]Kisha Yakobo akambariki Farao, naye akaondoka mbele ya uso wake.

11 [k]Ndipo Yosefu akawawakalisha baba yake na ndugu zake katika nchi ya Misri na kuwapa milki katika sehemu bora sana ya nchi, wilaya ya Ramesesi, kama Farao alivyoelekeza. 12 [l]Pia Yosefu akampa baba yake, na ndugu zake na wote wa nyumbani mwa baba yake vyakula, kwa kulingana na hesabu ya watoto wao.

### *Uongozi Wa Yosefu Wakati Wa Njaa*

13 [m]Hata hivyo, hapakuwepo chakula katika sehemu yote kwa kuwa njaa ilikuwa kali sana; Misri na Kanaani zote zikaharibiwa kwa sababu ya njaa. 14 [n]Yosefu akakusanya fedha zote zilizopatikana kutoka mauzo ya nafaka huko Misri na Kanaani, akazileta kwenye jumba la kifalme la Farao. 15 [o]Fedha za watu wa Misri na Kanaani zilipokwisha, Wamisri wote wakamjia Yosefu na kumwambia, "Tupatie chakula. Kwa nini tufe mbele ya macho yako? Fedha zetu zimekwisha."

16 [p]Yosefu akawaambia, "Basi leteni mifugo yenu, nitawauzia chakula kwa kubadilisha na mifugo yenu, kwa kuwa fedha zenu zimekwisha." 17 [q]Kwa hiyo wakaleta mifugo yao kwa Yosefu, naye akawapa chakula kwa kubadilishana na farasi zao, kondoo na mbuzi zao, ng'ombe na punda zao. Katika mwaka huo wote Yosefu akawapa chakula kwa kubadilishana na mifugo yao yote.

---

[a]**46:32** Mwa 42:20
[b]**46:33** Mwa 47:3
[c]**46:34** Mwa 43:32
[d]**47:1** Mwa 46:31
[e]**47:3** Mwa 46:33
[f]**47:4** Mwa 46:34
[g]**47:6** Kut 18:21
[h]**47:7** 2Sam 14:22
[i]**47:9** Mwa 25:7
[j]**47:10** Mwa 47:7
[k]**47:11** Hes 33:3, 5
[l]**47:12** Mwa 45:11
[m]**47:13** Mwa 12:10
[n]**47:14** Kut 7:23
[o]**47:15** Kut 16:3
[p]**47:16** Mwa 47:18, 19
[q]**47:17** Kut 14:9

18 Mwaka ule ulipokwisha, wakamjia
mwaka uliofuata na kumwambia,
“Hatuwezi kuficha ukweli mbele za bwana
wetu kwamba, kwa kuwa fedha zetu
zimekwisha na wanyama wetu ni mali
yako, sasa hakuna chochote kilichosalia
kwa ajili ya bwana wetu isipokuwa miili
yetu na ardhi yetu. 19 Kwa nini tuangamie
mbele ya macho yako, sisi pamoja na nchi
yetu? Utununue sisi pamoja na ardhi yetu
ili kubadilishana kwa chakula. Nasi pamoja
na nchi yetu tutakuwa watumwa wa Farao.
Tupe sisi mbegu ili tuweze kuishi wala
tusife, nchi yetu isije ikawa ukiwa.”

20 [a]Kwa hiyo Yosefu akamnunulia Farao
nchi yote ya Misri. Wamisri, mmoja
baada ya mwingine, waliuza mashamba
yao, kwa sababu njaa ilikuwa kali sana
kwao. Nchi ikawa mali ya Farao, 21 naye
Yosefu akawafanya watu watumike kama
watumwa, kuanzia upande mmoja wa
Misri hadi upande mwingine. 22 [b]Hata
hivyo, hakununua nchi ya makuhani, kwa
sababu walikuwa wanapata mgawo wao wa
kawaida kutoka kwa Farao, nao walikuwa
na chakula cha kuwatosha kutokana na
mgawo waliopewa na Farao. Hii ndiyo
sababu hawakuuza ardhi yao.

23 [c]Yosefu akawaambia watu, “Kwa vile
nimewanunua ninyi pamoja na nchi yenu leo
kuwa mali ya Farao, hapa kuna mbegu kwa
ajili yenu ili mweze kuziotesha. 24 [d]Lakini
wakati mazao yatakapokuwa tayari, mpeni
Farao sehemu ya tano. Sehemu hizo nne
zitakazobaki mtaziweka kama mbegu kwa
ajili ya mashamba na kwa ajili ya chakula
chenu wenyewe na cha watu wa nyumbani
mwenu na watoto wenu.”

25 [e]Wakamwambia, “Umeokoa maisha
yetu. Basi na tupate kibali mbele ya macho
ya bwana wetu; tutakuwa watumwa wa
Farao.”

26 [f]Basi Yosefu akaiweka iwe sheria
kuhusu nchi ya Misri, ambayo inatumika
mpaka leo, kwamba, sehemu ya tano
ya mazao ni mali ya Farao. Ni nchi ya
makuhani tu ambayo haikuwa ya Farao.

27 [g]Basi Waisraeli wakaishi Misri katika
nchi ya Gosheni. Wakapata mali huko
wakastawi na kuongezeka kwa wingi sana.

28 [h]Yakobo akaishi Misri miaka kumi na
saba, nayo miaka ya maisha yake ilikuwa
147. 29 [i]Wakati ulipokaribia wa Israeli kufa,
akamwita mwanawe Yosefu na kumwambia,
“Kama nimepata kibali machoni pake, weka
mkono wako chini ya paja langu na uniahidi
kuwa utanifanyia fadhili na uaminifu.
Usinizike Misri, 30 [j]lakini nitakapopumzika
na baba zangu, unichukue kutoka Misri,
ukanizike walipozikwa.”

Yosefu akamwambia, “Nitafanya kama
unavyosema.”

31 [k]Akamwambia, “Niapie.” Ndipo Yosefu
akamwapia, naye Israeli akaabudu, akiwa
ameegemea juu ya kichwa cha fimbo yake.

### *Manase Na Efraimu*

48 [l]Baada ya muda Yosefu akaambiwa
kwamba, “Baba yako ni mgonjwa.”
Kwa hiyo akawachukua wanawe wawili
Manase na Efraimu, pamoja naye. 2 [m]Yakobo
alipoambiwa, “Mwanao Yosefu amekujia
kukuona,” Israeli akakusanya nguvu zake,
akaketi kitandani.

3 [n]Yakobo akamwambia Yosefu, “Mungu
Mwenyezi[o] alinitokea huko Luzu katika
nchi ya Kanaani, huko akanibariki,
4 [p]naye akaniambia, ‘Nitakufanya ustawi
na kuongezeka hesabu yako, nitakufanya
kuwa jamii ya mataifa, nami nitakupa nchi
hii uimiliki milele wewe na wazao wako
baada yako.’

---

[a]**47:20** Mwa 12:10
[b]**47:22** Kum 14:28-29
[c]**47:23** Neh 5:3
[d]**47:24** Mwa 41:34
[e]**47:25** Mwa 32:5
[f]**47:26** Mwa 41:34
[g]**47:27** Mwa 1:22
[h]**47:28** Za 105:23
[i]**47:29** Mwa 24:32
[j]**47:30** Yos 24:32
[k]**47:31** Amu 15:12
[l]**48:1** Mwa 41:52; Ebr 11:2
[m]**48:2** Mwa 48:8-9
[n]**48:3** Mwa 17:1; 28:13
[o]3 Mungu Mwenyezi hapa ni jina la Kiebrania, El-Shaddai (yaani Mungu Mwenye utoshelevu wote).
[p]**48:4** Mwa 12:2; 15:7

5 [a]“Sasa basi, wanao wawili waliozaliwa
kwako huku Misri kabla sijaja hapa
kwako watahesabiwa kuwa ni wangu;
Efraimu na Manase watakuwa wangu,
kama vile Reubeni na Simeoni walivyo
wangu. 6 Lakini watoto utakaowazaa
baada yao watakuwa wako. Katika nchi
watakayoirithi, watatambuliwa kwa jina
la ndugu zao. 7 [b]Nilipokuwa ninarudi kutoka
Padani, katika huzuni yangu Raheli alifariki
katika nchi ya Kanaani tulipokuwa tungali
tukisafiri, tukiwa karibu kufika Efrathi. Kwa
hiyo nilimzika huko, kando ya njia iendayo
Efrathi” (yaani Bethlehemu).
8 [c]Wakati Israeli alipowaona wana wa
Yosefu, akauliza, “Hawa ni nani?”
9 [d]Yosefu akamjibu baba yake, “Hawa ni
wana ambao Mungu amenipa nikiwa huku.”
Ndipo Israeli akasema, “Walete kwangu
ili niwabariki.”
10 [e]Basi macho ya Israeli yalikuwa hayaoni
vizuri kwa sababu ya uzee, naye aliona kwa
shida. Kwa hiyo Yosefu akawaleta wanawe
karibu na baba yake, Israeli akawabusu na
akawakumbatia.
11 [f]Israeli akamwambia Yosefu, “Kamwe
sikutazamia kuuona uso wako tena, lakini
sasa Mungu ameniruhusu kuwaona watoto
wako pia.”
12 Ndipo Yosefu akawaondoa wanawe
magotini mwa Israeli naye akasujudu
hadi nchi. 13 [g]Yosefu akachukua wale wana
wawili, Efraimu kwenye mkono wake
wa kuume akimwelekeza kwenye mkono
wa kushoto wa Israeli, na Manase katika
mkono wake wa kushoto akimwelekeza
kwenye mkono wa kuume wa Israeli,
akawaleta karibu na babu yao. 14 Lakini
Israeli akaupeleka mkono wake wa kuume,
akauweka juu ya kichwa cha Efraimu,
ingawa alikuwa ndiye mdogo, na mkono
wake wa kushoto akaukatisha, akauweka
juu ya kichwa cha Manase, ingawa Manase
alikuwa ndiye mzaliwa wa kwanza.
15 Ndipo akambariki Yosefu akisema,

“Mungu ambaye baba zangu
Abrahamu na Isaki walimtii,
Mungu ambaye amekuwa mchungaji
wa maisha yangu yote mpaka leo
hii,
16 [h]Malaika ambaye aliniokoa kutoka
madhara yote,
yeye na awabariki vijana hawa.
Na waitwe kwa jina langu
na kwa majina ya baba zangu
Abrahamu na Isaki,
wao na waongezeke kwa wingi
katika dunia.”

17 [i]Yosefu alipoona baba yake akiweka
mkono wa kuume juu ya kichwa cha
Efraimu, hakupendezwa, kwa hiyo
akauchukua mkono wa baba yake kutoka
kichwa cha Efraimu na kuuweka juu ya
kichwa cha Manase. 18 [j]Yosefu akamwambia,
“Hapana, baba yangu, huyu ndiye mzaliwa
wa kwanza; uweke mkono wako wa kuume
juu ya kichwa chake.”
19 [k]Lakini baba yake akakataa, akasema,
“Ninajua, mwanangu, ninajua. Yeye pia
atakuwa taifa, naye pia atakuwa mkuu. Hata
hivyo, ndugu yake mdogo atakuwa mkuu
kuliko yeye, nao wazao wake watakuwa
kundi la mataifa.” 20 [l]Akawabarikia siku ile
na kusema,

“Kwa jina lenu Israeli watatamka
baraka hii:
‘Mungu na awafanye kama
Efraimu na Manase.’ ”

Kwa hiyo akamtanguliza Efraimu mbele
ya Manase.
21 [m]Ndipo Israeli akamwambia Yosefu,
“Mimi ninakaribia kufa, lakini Mungu
atakuwa pamoja nanyi, na atawarudisha

---

[a]**48:5** Mwa 41:50-52; 29:32
[b]**48:7** Mwa 35:19; Rut 1:2
[c]**48:8** Mwa 48:2
[d]**48:9** Mwa 33:5; 24:60
[e]**48:10** Mwa 27:1; 29:13
[f]**48:11** Mwa 44:28; 50:23
[g]**48:13** Za 16:8; Mt 25:33
[h]**48:16** Yer 15:21; Ebr 11:21
[i]**48:17** Mwa 48:14
[j]**48:18** Mwa 48:14
[k]**48:19** Mwa 25:23; 12:2
[l]**48:20** Mwa 24:60
[m]**48:21** Mwa 26:3; 28:13

katika nchi ya baba zenu. 22 [a]Kwako wewe, kama aliye juu ya ndugu zako, ninakupa sehemu moja zaidi ya ndugu zako, lile eneo nililoteka kwa Waamori kwa upanga wangu na upinde wangu."

*Yakobo Abariki Wanawe*

49 [b]Ndipo Yakobo akawaita wanawe na kusema: "Kusanyikeni kunizunguka ili niweze kuwaambia lile litakalowatokea siku zijazo.

2 [c]"Kusanyikeni na msikilize, enyi
wana wa Yakobo,
msikilizeni baba yenu Israeli.

3 [d]"Reubeni, wewe ni mzaliwa wangu
wa kwanza,
nguvu zangu, tunda la kwanza la
nguvu zangu,
umepita kwa heshima, umepita
kwa uwezo.
4 Usiyezuiwa kama maji, basi
hutakuwa mkuu tena,
kwa kuwa ulipanda kwenye
kitanda cha baba yako,
kwenye kitanda changu na
kukinajisi.

5 [e]"Simeoni na Lawi ni wana ndugu:
panga zao ni silaha za jeuri.
6 [f]Mimi na nisiingie katika baraza lao,
nami nisiunganike katika
kusanyiko lao,
kwa kuwa wamewaua watu katika
hasira yao,
walikata mishipa ya miguu ya
mafahali
kama walivyopenda.
7 [g]Hasira yao na ilaaniwe, kwa kuwa
ni kali mno,
nayo ghadhabu yao ni ya ukatili!
Nitawatawanya katika Yakobo
Na kuwasambaza katika Israeli.

8 [h]"Yuda, ndugu zako watakusifu;
mkono wako utakuwa shingoni
mwa adui zako;
wana wa baba yako
watakusujudia.
9 [i]Ee Yuda, wewe ni mwana simba;
unarudi toka mawindoni,
mwanangu.
Kama simba hunyemelea na kulala
chini,
kama simba jike: nani athubutuye
kumwamsha?
10 [j]Fimbo ya ufalme haitaondoka kwa
Yuda,
wala fimbo ya mtawala kati ya
miguu yake,
hadi aje yeye ambaye milki ni yake,
ambaye utii wa mataifa ni wake.
11 Atamfunga punda wake katika
mzabibu,
naye mwana-punda wake kwenye
tawi lililo bora zaidi;
atafua mavazi yake katika divai,
majoho yake katika damu ya
mizabibu.
12 Macho yake yatakuwa mekundu kwa
divai,
meno yake yatakuwa meupe kwa
maziwa.

13 [k]"Zabuloni ataishi pwani ya bahari
na kuwa bandari za kuegesha
meli;
mpaka wake utapanuka kuelekea
Sidoni.

14 "Isakari ni punda mwenye nguvu
ambaye amelala kati ya mizigo
yake.
15 [l]Aonapo palivyo pazuri mahali pake
pa kupumzika
na jinsi nchi yake inavyopendeza,
atainamisha bega lake kwenye mzigo
na kujitolea kwa ajili ya kazi
ngumu.

---

[a]**48:22** Yos 24:32; Yn 4:5
[b]**49:1** Hes 24:14; Kum 31:29
[c]**49:2** Yos 24:1; Za 34:11
[d]**49:3** Mwa 29:32; Kum 21:17; Za 78:51
[e]**49:5** Mwa 29:33; Mit 4:17
[f]**49:6** Mit 1:15; Efe 5:11
[g]**49:7** Yos 19:1, 9; Mwa 29:35
[h]**49:8** 1Nya 5:2; Kum 28:48
[i]**49:9** Hes 24:9; Ay 38:39
[j]**49:10** Eze 21:27; Isa 42:1
[k]**49:13** Mwa 30:20; 10:19
[l]**49:15** Yos 19:17-23; Eze 29:18

[16] "Dani atahukumu watu wake kwa
haki
kama mmoja wa makabila ya
Israeli.
[17] [a]Dani atakuwa nyoka kando ya
barabara,
nyoka mwenye sumu kando ya
njia,
yule aumaye visigino vya farasi
ili yule ampandaye aanguke chali.

[18] "Ee BWANA, nautafuta wokovu
wako.

[19] "Gadi atashambuliwa ghafula na
kundi la washambuliaji,
lakini yeye atawageukia na
kuwashinda kabisa.

[20] [b]"Chakula cha Asheri kitakuwa
kinono,
naye atatoa chakula kitamu
kimfaacho mfalme.

[21] "Naftali ni kulungu jike aliyeachiwa
huru
azaaye watoto wazuri.

[22] [c]"Yosefu ni mzabibu uzaao,
mzabibu uzaao ulio kando ya
chemchemi,
ambao matawi yake hutanda
ukutani.
[23] Kwa uchungu wapiga mshale
walimshambulia,
wakampiga mshale kwa ukatili.
[24] [d]Lakini upinde wake ulibaki imara,
mikono yake ikatiwa nguvu,
na mkono wa Mwenye Nguvu wa
Yakobo,
kwa sababu ya Mchungaji,
Mwamba wa Israeli,
[25] [e]kwa sababu ya Mungu wa baba
yako, anayekusaidia,
kwa sababu ya Mwenyezi,[f] yeye
anayekubariki
kwa baraka za mbinguni juu,
baraka za kilindi kilichoko chini,
baraka za matitini na za tumbo la
uzazi.
[26] Baraka za baba yako ni kubwa
kuliko baraka za milima ya kale,
nyingi kuliko vilima vya kale.
Baraka hizo zote na zikae juu ya
kichwa cha Yosefu,
juu ya paji la yule mkuu miongoni
mwa ndugu zake.

[27] [g]"Benyamini ni mbwa mwitu mlafi
mwenye njaa kuu;
asubuhi hurarua mawindo yake,
jioni hugawa nyara."

[28] Haya yote ndiyo makabila kumi na
mawili ya Israeli, na hivi ndivyo baba yao
alivyowaambia alipowabariki, akimpa kila
mmoja baraka inayomfaa.

*Kifo Cha Yakobo*

[29] [h]Ndipo alipowapa maelekezo haya:
"Mimi niko karibu kukusanywa kwa watu
wangu. Mnizike pamoja na baba zangu
kwenye pango katika shamba la Efroni,
Mhiti, [30] pango lililoko katika shamba la
Makpela, karibu na Mamre huko Kanaani,
ambalo Abrahamu alinunua kwa ajili ya
mahali pa kuzikia kutoka kwa Efroni,
Mhiti, pamoja na shamba. [31] [i]Huko ndiko
Abrahamu na Sara mkewe walikozikwa,
huko akazikwa Isaki na Rebeka mkewe,
na huko nilimzika Lea. [32] Shamba hilo
na pango lililoko ndani yake lilinunuliwa
kutoka kwa Wahiti."
[33] [j]Baada ya Yakobo kumaliza kutoa
maelekezo hayo kwa wanawe, akarudisha
miguu yake kitandani, akapumua pumzi ya
mwisho, na akakusanywa kwa watu wake.
50 Basi Yosefu akamwangukia baba
yake, akalilia juu yake na akambusu.
[2] [k]Ndipo Yosefu akawaagiza matabibu
waliokuwa wakimhudumia, wamtie baba
yake Israeli dawa ili asioze. Hivyo matabibu

---

[a]**49:17** Amu 18:27; Yer 8:17
[b]**49:20** Mwa 30:13; Isa 25:6; Ay 29:6
[c]**49:22** Mwa 30:24; Eze 19:10
[d]**49:24** Za 18:34; Isa 1:24
[e]**49:25** Kut 18:4; Mwa 27:28
[f]25 Mwenyezi hapa ina maana ya Shaddai kwa Kiebrania.
[g]**49:27** Amu 20:12-13; Ebr 1:8; Hes 31:11
[h]**49:29** Mwa 25:8; 2Sam 2:32
[i]**49:31** Mwa 25:9; 23:19
[j]**49:33** Mwa 25:8; Mdo 7:15
[k]**50:2** Mwa 50:26; 2Nya 16:14

wakamtia dawa asioze, 3 [a]wakatumia siku
arobaini, kwa maana ndio muda uliotakiwa
wa kutia dawa ili asioze. Nao Wamisri
wakamwombolezea Yakobo kwa siku
sabini.
4 [b]Siku za kumwombolezea zilipokwisha,
Yosefu akawaambia washauri wa Farao,
“Kama nimepata kibali machoni penu
semeni na Farao kwa ajili yangu.
Mwambieni, 5 [c]‘Baba yangu aliniapisha na
kuniambia, “Mimi niko karibu kufa; unizike
katika kaburi lile nililochimba kwa ajili
yangu mwenyewe katika nchi ya Kanaani.”
Sasa nakuomba uniruhusu niende kumzika
baba yangu, nami nitarudi.’ ”
6 Farao akasema, “Panda, uende kumzika
baba yako, kama alivyokuapiza kufanya.”
7 [d]Hivyo Yosefu akapanda kwenda
kumzika baba yake. Maafisa wote wa Farao
wakaenda pamoja naye, watu mashuhuri
wa baraza lake na watu mashuhuri wote
wa Misri. 8 Hawa ni mbali na watu wote wa
nyumbani kwa Yosefu, na ndugu zake, na
wale wote wa nyumbani mwa baba yake.
Ni watoto wao, makundi yao ya kondoo,
mbuzi na ng’ombe tu waliobakia katika
nchi ya Gosheni. 9 [e]Magari makubwa na
wapanda farasi pia walipanda pamoja naye.
Likawa kundi kubwa sana.
10 [f]Walipofika kwenye sakafu ya kupuria
nafaka ya Atadi, karibu na Yordani,
wakalia kwa sauti na kwa uchungu;
Yosefu akapumzika huko kwa siku saba
kumwombolezea baba yake. 11 [g]Wakanaani
walioishi huko walipoona maombolezo
yaliyofanyika katika sakafu ile ya kupuria
ya Atadi, wakasema, “Wamisri wanafanya
maombolezo makubwa.” Kwa hiyo
mahali pale karibu na Yordani pakaitwa
Abel-Mizraimu.[h]
12 Hivyo wana wa Yakobo wakafanya
kama baba yao alivyowaagiza:
13 [i]Wakamchukua mpaka nchi ya Kanaani,
wakamzika kwenye pango katika shamba
la Makpela, karibu na Mamre, ambalo
Abrahamu alilinunua kutoka kwa Efroni,
Mhiti, pamoja na shamba liwe mahali pa
kuzikia. 14 Baada ya Yosefu kumzika baba
yake, akarudi Misri pamoja na ndugu zake
na wale wote waliokuwa wamekwenda
naye kumzika baba yake.

*Yosefu Awaondolea Ndugu Zake Mashaka*

15 [j]Ndugu zake Yosefu walipoona kwamba
baba yao amekufa, wakasema, “Itakuwaje
kama Yosefu ataweka kinyongo dhidi yetu
na kutulipa mabaya yote tuliyomtendea?”
16 Kwa hiyo wakampelekea Yosefu ujumbe,
wakasema, “Kabla baba yako hajafa
aliacha maagizo haya: 17 [k]‘Hili ndilo
mtakalomwambia Yosefu: Ninakuomba
uwasamehe ndugu zako dhambi na mabaya
kwa vile walivyokutenda vibaya.’ Sasa
tafadhali samehe dhambi za watumishi
wa Mungu wa baba yako.” Ujumbe huu
ulipomfikia, Yosefu akalia.
18 [l]Ndipo ndugu zake wakaja na kujitupa
chini mbele yake. Wakasema, “Sisi ni
watumwa wako.”
19 [m]Lakini Yosefu akawaambia, “Msiogope.
Je, mimi ni badala ya Mungu? 20 [n]Mlikusudia
kunidhuru, lakini Mungu alikusudia mema,
ili litimie hili linalofanyika sasa, kuokoa
maisha ya watu wengi. 21 [o]Hivyo basi,
msiogope. Mimi nitawatunza ninyi nyote
pamoja na watoto wenu.” Akawahakikishia
na kusema nao kwa wema.

*Kifo Cha Yosefu*

22 [p]Yosefu akakaa katika nchi ya Misri,
yeye pamoja na jamaa yote ya baba
yake. Akaishi miaka 110, 23 naye akaona
kizazi cha tatu cha watoto wa Efraimu.

[a]**50:3** Kum 1:3; Mwa 30:27
[b]**50:4** Mwa 27:41
[c]**50:5** Mwa 24:37; 2Sam 18:18
[d]**50:7** Mwa 45:16
[e]**50:9** Mwa 41:43
[f]**50:10** Hes 15:20; 1Sam 31:13
[g]**50:11** Mwa 10:18; 37:34
[h]11 Abel-Mizraimu maana yake Maombolezo ya Wamisri.
[i]**50:13** Mwa 23:20
[j]**50:15** Mwa 37:28
[k]**50:17** Mt 6:14; Mwa 29:11
[l]**50:18** Mwa 37:7
[m]**50:19** Rum 12:19; Ebr 10:30
[n]**50:20** Rum 8:28; Mwa 45:5
[o]**50:21** Mwa 45:11; Efe 4:32
[p]**50:22** Mwa 25:7; Yos 24:29

Pia akaona watoto wa Makiri mwana wa
Manase, wakawekwa magotini mwa Yosefu
walipozaliwa.

24 [a]Ndipo Yosefu akawaambia ndugu zake,
“Mimi ninakaribia kufa. Lakini kwa hakika
Mungu atawasaidia na kuwachukueni
kutoka nchi hii na kuwapeleka katika nchi
aliyomwahidi kwa kiapo Abrahamu, Isaki
na Yakobo.” 25 Naye Yosefu akawaapisha
wana wa Israeli na kuwaambia, “Hakika
Mungu atawasaidia, nanyi ni lazima
mhakikishe mmepandisha mifupa yangu
kutoka mahali hapa.”

26 Kwa hiyo Yosefu akafa akiwa na umri
wa miaka 110. Baada ya kumtia dawa ili
asioze, akawekwa kwenye jeneza huko
Misri.

[a]**50:24** Rut 1:6; Za 35:2; Mwa 12:7

# KUTOKA

*Waisraeli Waonewa*

1 [a]Haya ndiyo majina ya wana wa Israeli
ambao walikwenda Misri na Yakobo,
kila mmoja akiwa pamoja na jamaa yake:
2 Reubeni, Simeoni, Lawi na Yuda; 3 Isakari,
Zabuloni na Benyamini; 4 [b]Dani na Naftali,
Gadi na Asheri. 5 [c]Wazao wote wa Yakobo
walikuwa watu sabini; Yosefu alikuwa
tayari yuko Misri.
6 [d]Basi Yosefu na kaka zake wote na kizazi
kile chote walikufa, 7 [e]lakini Waisraeli
walikuwa wamezaana na kuongezeka sana,
idadi yao ikawa kubwa mno, kwa hiyo
wakaijaza nchi.
8 [f]Kisha mfalme mpya ambaye
hakufahamu habari za Yosefu akatawala
Misri. 9 [g]Akawaambia watu wake,
"Tazameni, Waisraeli wamekuwa wengi
mno kwa idadi kutuliko sisi. 10 [h]Njooni, ni
lazima tuwashughulikie kwa uangalifu, la
sivyo watazidi kuwa wengi zaidi, na ikiwa
patatokea vita, watajiunga na adui zetu
kupigana dhidi yetu na kuondoka katika
nchi hii."
11 [i]Basi Wamisri wakaweka wasimamizi
wa kuwasimamia na kuwatesa Waisraeli
kwa kazi ngumu, nao wakajenga miji ya
Pithomu na Ramesesi ya kuweka akiba ya
Farao. 12 Lakini walivyozidi kuteswa ndivyo
walivyozidi kuongezeka na kuenea katika
nchi; Wamisri wakawaogopa Waisraeli,
13 [j]kwa hiyo wakawatumikisha kwa ukatili.
14 [k]Wakafanya maisha ya Waisraeli kuwa
machungu kwa kufanya kazi ngumu ya
kutengeneza lami na kufyatua matofali,
na kazi zote za mashambani; katika kazi
zao zote ngumu, Wamisri waliwatumia
Waisraeli kwa ukatili.
15 [l]Mfalme wa Misri akawaambia wakunga
wa Kimisri waliowazalisha wanawake wa
Kiebrania, ambao majina yao ni Shifra na
Pua, 16 "Mtakapowazalisha wanawake wa
Kiebrania, chunguzeni wanapojifungua.
Ikiwa ni mtoto wa kiume, muueni, lakini
ikiwa ni msichana, mwacheni aishi."
17 [m]Lakini hao wakunga walimcha Mungu
na hawakufanya kile mfalme wa Misri
alichowaambia kufanya, bali wakawaacha
watoto wa kiume waishi. 18 Ndipo
mfalme wa Misri akawaita hao wakunga,
akawauliza, "Kwa nini mmefanya hivi?
Mbona mmeacha watoto wa kiume waishi?"
19 [n]Wakunga wakamjibu Farao,
"Wanawake wa Kiebrania ni tofauti na
wanawake wa Kimisri; wao wana nguvu,
nao hujifungua watoto kabla wakunga
hawajafika."
20 [o]Kwa hiyo Mungu akawatendea mema
wakunga hao. Waisraeli wakaongezeka na
kuendelea kuwa wengi zaidi. 21 [p]Kwa vile
hao wakunga walimcha Mungu, Mungu
akawajalia kuwa na jamaa zao wenyewe.
22 [q]Kisha Farao akatoa agizo hili kwa
watu wake wote: "Kila mtoto wa kiume
atakayezaliwa kwa Waebrania lazima

[a]**1:1** Mwa 46:8
[b]**1:4** Mwa 35:22-26; Hes 1:20-43
[c]**1:5** Mwa 46:26
[d]**1:6** Mwa 50:26; Mdo 7:15
[e]**1:7** Mwa 12:2; Kum 7:13; Eze 16:7
[f]**1:8** Yer 43:11; 46:2
[g]**1:9** Mwa 26:16
[h]**1:10** Mwa 15:13; Kut 3:7; 18:11; Za 64:2; 71:10; 83:3; 105:24-25; Isa 53:3; Mdo 7:17-19
[i]**1:11** Kut 3:7; 5:4, 10-14; 6:6-7; 2:11; Mwa 15:13; 47:11; Yos 9:27; Isa 60:10; 1Fal 9:19, 21; 1Nya 22:2; 2Nya 8:4
[j]**1:13** Mwa 15:13-14; Kut 5:21; 16:3; Law 25:43-53; Kum 4:20; 26:6; 1Fal 8:15; Za 129:1; Isa 30:6; 48:10; Yer 11:4
[k]**1:14** Kum 26:6; Ezr 9:9; Isa 14:3; Mwa 11:3; Kut 2:23; 3:9; Hes 20:15; Mdo 7:19; 1Sam 10:11; 2Sam 13:4
[l]**1:15** Mwa 35:17
[m]**1:17** Mit 16:6; 1Sam 22:17; Dan 3:16-18; Mdo 4:18-20; 5:29
[n]**1:19** Law 19:11; Yos 2:4-6; 1Sam 19:14; 2Sam 17:20
[o]**1:20** Mit 11:18; 22:8; Mhu 8:12; Isa 3:10; Ebr 6:10
[p]**1:21** 1Sam 2:35; 2Sam 7:11, 27-29; 1Fal 11:38; 14:10
[q]**1:22** Mwa 41:1; Mdo 7:19

atupwe katika Mto Naili, bali kila mtoto
wa kike aachwe aishi.”

*Kuzaliwa Kwa Mose*

2 [a]Basi mtu mmoja wa nyumba ya Lawi
akaoa mwanamke Mlawi, 2 [b]naye
mwanamke huyo akapata mimba, akazaa
mtoto wa kiume. Alipoona mtoto huyo
ni mzuri, akamficha kwa miezi mitatu.
3 [c]Lakini alipoona hawezi kumficha zaidi,
akamtengenezea kisafina cha mafunjo,
akakipaka lami. Kisha akamweka huyo
mtoto ndani yake, akakificha katikati ya
matete kando ya ukingo wa Mto Naili.
4 [d]Dada ya huyo mtoto akasimama mbali
ili kuona kitakachompata mtoto.

5 [e]Ndipo binti Farao akateremka mtoni
Naili kuoga, nao wahudumu wake
wakawa wanatembea ukingoni mwa mto.
Binti mfalme akaona kisafina katikati ya
manyasi, akamtuma mmoja wa watumwa
wake wa kike kukichukua. 6 Alifungua
kisafina akaona mtoto ndani yake. Mtoto
alikuwa akilia, akamhurumia. Akasema,
“Huyu ni mmoja wa watoto wa Kiebrania.”

7 Ndipo dada wa huyo mtoto akamuuliza
binti Farao, “Je, niende nikakutafutie
mmoja wa wanawake wa Kiebrania akulelee
huyu mtoto?”

8 Binti Farao akamjibu, “Ndiyo, nenda.”
Yule msichana akaenda akamleta mama
wa mtoto. 9 Binti Farao akamwambia,
“Mchukue huyu mtoto unisaidie kumlea,
nami nitakulipa.” Basi yule mwanamke
akamchukua mtoto na kumlea. 10 [f]Mtoto
alipokua, akampeleka kwa binti Farao, naye
akawa mwanawe. Akamwita jina lake Mose
akisema, “Nilimtoa kwenye maji.”

*Mose Akimbilia Midiani*

11 [g]Siku moja, baada ya Mose kukua,
akaondoka kwenda walikokuwa watu
wake, na akachunguza jinsi walivyokuwa
wakifanya kazi ngumu. Akamwona Mmisri
akimpiga Mwebrania, mmojawapo wa
watu wake. 12 Mose akatazama huku na
huko asione mtu yeyote, akamuua yule
Mmisri, akamficha mchangani. 13 [h]Kesho
yake akatoka, akaona Waebrania wawili
wakipigana. Akamuuliza yule aliyekosa,
“Mbona unampiga Mwebrania mwenzako?”

14 [i]Yule mtu akamjibu, “Ni nani
aliyekufanya mtawala na mwamuzi juu
yetu? Je, unataka kuniua kama ulivyomuua
yule Mmisri?” Ndipo Mose akaogopa na
kuwaza, “Jambo lile nililofanya lazima
limefahamika.”

15 [j]Farao aliposikia jambo hili, alijaribu
kumuua Mose, lakini Mose akamkimbia
Farao na kwenda kuishi katika nchi ya
Midiani, akaketi kando ya kisima. 16 [k]Kuhani
wa Midiani alikuwa na binti saba, nao
wakaja kisimani ili kuchota maji na kujaza
hori kwa ajili ya kunyweshea mifugo ya
baba yao. 17 [l]Baadhi ya wachungaji wakaja
wakawafukuza hao wasichana. Ndipo Mose
akainuka, akawasaidia na kunywesha
mifugo yao.

18 [m]Hao wasichana waliporudi nyumbani
kwa Reueli baba yao, akawauliza,
“Imekuwaje leo mmerudi mapema hivyo?”

19 Wakamjibu, “Mmisri mmoja alituokoa
kutoka mikononi mwa wachungaji. Pia
mtu huyo alituchotea maji na kunywesha
mifugo.”

20 [n]Akawauliza binti zake, “Yuko wapi?
Mbona mmemwacha? Mkaribisheni ale
chakula.”

21 [o]Mose akakubali kukaa kwa huyo mtu,
ambaye alimpa Mose binti yake aliyeitwa
Sipora amwoe. 22 [p]Sipora alizaa mtoto wa
kiume, naye Mose akamwita Gershomu,

---

[a]**2:1** Mwa 29:34; Kut 6:20; Hes 26:29
[b]**2:2** Mwa 39:6; Ebr 11:23
[c]**2:3** Isa 18:2; Mwa 6:14; 41:2; Ay 8:11; Mdo 7:21
[d]**2:4** Kut 15:20
[e]**2:5** Kut 7:15; 8:20
[f]**2:10** 1Sam 1:20; 2Sam 22:17
[g]**2:11** Mdo 7:23; Ebr 11:24-26; Kut 1:11
[h]**2:13** Mdo 7:26
[i]**2:14** Mwa 13:8; Mdo 7:27
[j]**2:15** Kut 4:19; Ebr 11:27; Mwa 31:21
[k]**2:16** Kut 3:1; 18:1; Mwa 24:11
[l]**2:17** 1Sam 30:8; Za 31:2; Mwa 29:10
[m]**2:18** Kut 3:1; 4:18; 18:5-12; Hes 10:29
[n]**2:20** Mwa 18:2-5
[o]**2:21** Kut 4:25; 18:2; Hes 12:1
[p]**2:22** Amu 18:30; Mwa 23:4; Ebr 11:13

akisema, “Nimekuwa mgeni katika nchi ya
kigeni.”
23 [a]Baada ya muda mrefu, mfalme wa
Misri akafa. Waisraeli wakalia kwa huzuni
katika utumwa wao, walilia na kilio chao
cha kutaka msaada kwa ajili ya utumwa
kikamfikia Mungu. 24 [b]Mungu akasikia
kilio chao cha huzuni, akakumbuka Agano
alilofanya na Abrahamu pamoja na Isaki na
Yakobo. 25 [c]Kwa hiyo Mungu akawaangalia
Waisraeli na kuwahurumia.

*Mose Na Kichaka Kinachowaka Moto*

3 [de]Basi Mose alikuwa anachunga mifugo
ya Yethro mkwewe, kuhani wa Midiani.
Mose akapeleka mifugo mbali nyuma ya
jangwa, naye akafika Horebu, mlima
wa Mungu. 2 [f]Huko malaika wa BWANA
akamtokea Mose katika mwali wa moto
kutoka kichakani. Mose akaona kwamba
ingawa kile kichaka kilikuwa kinawaka
moto, kilikuwa hakiteketei. 3 Ndipo Mose
akawaza, “Nitageuka sasa nione kitu hiki
cha ajabu, nami nione ni kwa nini kichaka
hiki hakiteketei.”
4 [g]BWANA alipoona kuwa amegeuka ili
aone, Mungu akamwita kutoka ndani ya
kile kichaka, “Mose! Mose!”
Naye Mose akajibu, “Mimi hapa.”
5 [h]Mungu akamwambia, “Usikaribie
zaidi. Vua viatu vyako, kwa maana mahali
unaposimama ni patakatifu.” 6 [i]Kisha
akamwambia, “Mimi ni Mungu wa baba
yako, Mungu wa Abrahamu, Mungu
wa Isaki, na Mungu wa Yakobo.” Mose
aliposikia hayo, akafunika uso wake kwa
sababu aliogopa kumtazama Mungu.
7 [j]BWANA akamwambia, “Hakika
nimeona mateso ya watu wangu katika
Misri. Nimesikia kilio chao kwa sababu
ya wasimamizi wao, nami naguswa na
mateso yao. 8 [k]Basi nimeshuka niwaokoe
kutoka mkono wa Wamisri, niwatoe
na kuwapandisha kutoka nchi hiyo,
niwapeleke katika nchi nzuri na kubwa,
nchi itiririkayo maziwa na asali, nchi ya
Wakanaani, Wahiti, Waamori, Waperizi,
Wahivi na Wayebusi. 9 [l]Sasa kilio cha
Waisraeli kimenifikia, nami nimeona jinsi
Wamisri wanavyowatesa. 10 [m]Basi, sasa
nenda. Ninakutuma kwa Farao ili kuwatoa
watu wangu Waisraeli kutoka Misri.”
11 [n]Lakini Mose akamwambia Mungu,
“Mimi ni nani hata niende kwa Farao
kuwatoa Waisraeli nchini Misri?”
12 [o]Naye Mungu akasema, “Mimi
nitakuwa pamoja nawe. Hii itakuwa ishara
kwako kwamba ni Mimi nimekutuma:
Hapo utakapokuwa umewatoa watu Misri,
mtamwabudu Mungu katika mlima huu.”
13 [p]Mose akamwambia Mungu, “Ikiwa

---

[a]**2:23** Mdo 7:30; Kut 4:19; 1:14; 3:7-9; 6:5; Hes 20:15-16; Kum 26:7; Yak 5:4; Amu 2:18; 1Sam 12:8; Za 5:2; 18:6; 39:12; 81:7
[b]**2:24** Mwa 8:1; 9:15; 15:15; 17:4; 22:16-18; 26:3; 28:13-15; Kut 32:13; 2Fal 13:23; Za 105:10, 42; Yer 14:21
[c]**2:25** Kut 3:7; 4:31; Lk 1:25
[d]**3:1** Kut 2:16, 18; 17:6; 19:1-11; 33:6; 4:27; 18:5; 24:13
[e]**3:1** Kum 1:2-6; 4:10, 11-15; 5:2; 1Fal 19:8; Amu 1:16; Mal 4:4
[f]**3:2** Mwa 16:7; Kut 2:2-6; 19:18; 4:5; Kum 5:19; 29:1; 1Fal 19:12; Kum 33:16; Mk 12:26; Lk 20:37; Mdo 7:30
[g]**3:4** Kut 19:3; 4:5; Mwa 31:11; 1Sam 3:4; Isa 6:8
[h]**3:5** Yer 30:21; Mwa 28:17; Mdo 7:33
[i]**3:6** Mwa 24:12; Kut 5:4; 24:11; 33:20; Mt 22:32; Mk 12:26; Lk 20:37; Mdo 3:13; 7:32; 1Fal 19:13; Amu 13:22; Ay 13:11; 23:16; 30:15; Isa 6:5
[j]**3:7** 1Sam 1:11; 9:16; Mwa 16:11; Neh 9:9; Za 106:44; Kut 2:25; Mdo 7:34
[k]**3:8** Mwa 11:5; 12:7; 15:14; Mdo 7:34; Kut 13:5; 33:3; Law 20:24; Hes 13:27; Kum 1:25; 6:3; 8:7-9; 11:9; 26:9; 27:3; Yos 5:6; 11:3; Yer 11:5; 32:22; Eze 20:6; Amu 3:3
[l]**3:9** Kut 1:14; Hes 10:9
[m]**3:10** Kut 4:12; 6:13, 26; 12:41, 51; 20:2; Yos 24:5; Mdo 7:34; 1Sam 12:6, 8; Za 105:26; Kum 4:20; 1Fal 8:16; Mik 6:4
[n]**3:11** Kut 4:10; 6:12, 30; Yer 1:6; Amu 6:15; 1Sam 9:21; 15:17; 18:18; 2Sam 7:18; 2Nya 2:6; Isa 6:5
[o]**3:12** Mwa 26:3; Kut 14:22; Rum 8:31; Hes 26:10; Yos 2:12; Amu 6:17; Za 86:17; Isa 7:14; 8:18; 20:3; Yer 44:29; Mdo 7:7
[p]**3:13** Mwa 32:29

nitawaendea Waisraeli na kuwaambia,
‘Mungu wa baba zenu amenituma kwenu,’
nao wakiniuliza, ‘Jina lake ni nani?’
Nitawaambia nini?”
14 [a]Mungu akamwambia Mose, “MIMI
NIKO AMBAYE NIKO. Hivyo ndivyo
utakavyowaambia Waisraeli: ‘MIMI NIKO
amenituma kwenu.’ ”
15 [b]Vilevile Mungu akamwambia Mose,
“Waambie Waisraeli, ‘BWANA, Mungu wa
baba zenu, Mungu wa Abrahamu, Mungu
wa Isaki, na Mungu wa Yakobo amenituma
kwenu.’ Hili ndilo Jina langu milele, Jina
ambalo mtanikumbuka kwalo kutoka kizazi
hadi kizazi.
16 [c]“Nenda, ukawakusanye wazee wa
Israeli, uwaambie, ‘BWANA, Mungu wa baba
zenu, Mungu wa Abrahamu, Isaki na Yakobo,
alinitokea akaniambia: Nimewatazama,
nami nimeona mliyofanyiwa katika
Misri. 17 [d]Nami nimeahidi kuwapandisha
kutoka mateso yenu katika nchi ya Misri,
niwapeleke nchi ya Wakanaani, Wahiti,
Waamori, Waperizi, Wahivi na Wayebusi,
nchi itiririkayo maziwa na asali.’
18 [e]“Wazee wa Israeli watakusikiliza.
Kisha wewe na wazee mtakwenda kwa
mfalme wa Misri na kumwambia, ‘BWANA,
Mungu wa Waebrania ametutokea.
Turuhusu twende safari ya siku tatu huko
jangwani kutoa dhabihu kwa BWANA
Mungu wetu.’ 19 [f]Lakini nafahamu kwamba
mfalme wa Misri hatawaruhusu kwenda,
mpaka mkono wenye nguvu umlazimishe.
20 [g]Kwa hiyo nitaunyoosha mkono wangu
na kuwapiga Wamisri kwa maajabu yote
nitakayofanya miongoni mwao. Baada ya
hayo, atawaruhusu mwondoke.
21 [h]“Nami nitawapa hawa watu upendeleo
mbele ya Wamisri, kwa hiyo mtakapoondoka
nchini hamtaondoka mikono mitupu.
22 [i]Kila mwanamke Mwisraeli atamwomba
jirani yake Mmisri na mwanamke yeyote
anayeishi nyumbani kwake ampe vyombo
vya fedha, dhahabu na nguo, ambavyo
mtawavika wana wenu na binti zenu. Hivyo
mtawateka nyara Wamisri.”

*Ishara Za Mose*

4 [j]Mose akamjibu, “Itakuwaje kama
hawataniamini au kunisikiliza, waseme,
‘BWANA hakukutokea’?”
2 [k]Ndipo BWANA akamwambia, “Ni nini
hicho kilicho mkononi mwako?”
Akajibu, “Fimbo.”
3 [l]BWANA akasema, “Itupe chini.”
Mose akaitupa chini hiyo fimbo nayo
ikawa nyoka, naye akaikimbia. 4 Kisha
BWANA akamwambia, “Nyoosha mkono
wako umkamate mkiani.” Basi Mose
akanyoosha mkono akamkamata yule
nyoka, naye akabadilika tena kuwa fimbo
mkononi mwake. 5 [m]BWANA akasema, “Hivi
ndivyo Waisraeli watakavyoamini kuwa
BWANA, Mungu wa baba zao, Mungu wa
Abrahamu, Mungu wa Isaki, na Mungu wa
Yakobo, amekutokea wewe.”

---

[a]**3:14** Kut 6:2-3; Yn 8:58; Ebr 13:8; Ufu 1:8; 4:8
[b]**3:15** Mwa 31:42; 24:12; Dan 2:23; Kut 6:3, 7; 15:3; 23:21; 34:5-7; Law 24:11; Kum 28:58; Za 30:4; 83:18; 96:2; 97:12; 135:13; 145:21; 45:17; 72:17; 102:12; Isa 42:8; Yer 16:21; 32:2; Hos 12:5
[c]**3:16** Kut 4:29, 31; 17:5; Law 4:15; Hes 16:25; 11:16; Kum 5:23; 19:12; Amu 8:14; Rut 4:2; Mit 31:23; Eze 8:11; Mwa 24:12; 2Fal 19:16; 2Nya 6:20; Za 33:18; 66:7
[d]**3:17** Mwa 15:16; 46:4; Kut 6:6
[e]**3:18** Kut 4:1, 8; 31:6; 6:12, 30; 4:23; 5:1-3; 6:11; 7:16; 9:13; 8:20, 27; 10:9, 26; Mwa 14:13; 30:26; Hes 23:4, 16
[f]**3:19** Kut 4:21; 6:6; 7:3; 10:1; 11:9; Kum 4:34; 2Nya 6:32
[g]**3:20** Kut 6:16; 7:4-5; 9:15; 13:3-9, 14-16; 11:1; 12:31-33; 4:21; 15:11; Kum 4:34; 5:15; 7:8; 26:8; 3:24; 6:22; 2Fal 17:36; 2Nya 6:32; Za 118:15-16; 136:12; 71:19; 72:18; 77:14; 78:43; 86:10; 105:27; 106:22; Isa 41:10; 63:12; Yer 21:5; 51:25; 30:20; Mik 7:15; Mdo 7:36; Dan 9:15; Hes 14:11; Neh 9:10
[h]**3:21** Mwa 39:21; Kut 11:2; 2Nya 30:9; Neh 1:11; Za 105:37; 106:46; Yer 42:12
[i]**3:22** Ay 27:16-17; Kut 11:2; 12:35; Ezr 1:4-6; 7:16; Mwa 15:14; Eze 39:10; 29:10; Za 105:37
[j]**4:1** Kut 3:18
[k]**4:2** Mwa 38:18; Kut 7:19; 8:5; 14:16, 21; 17:5-9; Hes 17:2; 20:8; Yos 8:18; Amu 6:21; 1Sam 14:27; 2Fal 4:29
[l]**4:3** Kut 7:8-15
[m]**4:5** Kut 3:6; 14:31; 19:9

6 [a]Kisha BWANA akamwambia, “Weka
mkono wako ndani ya joho lako.” Basi
Mose akaweka mkono wake ndani ya joho
lake, naye alipoutoa, ulikuwa na ukoma,
mweupe kama theluji.
7 [b]Mungu akamwambia, “Sasa urudishe
tena huo mkono ndani ya joho lako.” Basi
Mose akaurudisha mkono wake ndani ya
joho lake na alipoutoa, ulikuwa mzima,
kama sehemu zingine za mwili wake.
8 [c]Ndipo BWANA akamwambia, “Kama
hawatakuamini wewe, au kutojali ishara
ya kwanza, wataamini ishara ya pili.
9 [d]Lakini kama hawataamini ishara hizi
mbili au hawatawasikiliza ninyi, chukua
kiasi cha maji kutoka Mto Naili uyamimine
juu ya ardhi kavu. Maji mtakayotoa mtoni
yatakuwa damu juu ya ardhi.”
10 [e]Mose akamwambia BWANA, “Ee
Bwana, kamwe sijapata kuwa msemaji
kwa ufasaha wakati uliopita wala tangu
ulipoanza kuzungumza na mtumishi wako.
Ulimi wangu ni mzito kuzungumza.”
11 [f]BWANA akamwambia, “Ni nani
aliyempa mwanadamu kinywa? Ni nani
aliyemfanya mtu kuwa kiziwi au bubu? Ni
nani anayempa mtu kuona au upofu? Je, si
mimi, BWANA? 12 [g]Sasa nenda, nitakusaidia
kusema, nami nitakufundisha jambo la
kusema.”
13 [h]Lakini Mose akasema, “Ee Bwana,
tafadhali mtume mtu mwingine kufanya
kazi hiyo.”
14 [i]Ndipo hasira ya BWANA ikawaka dhidi
ya Mose, akamwambia, “Vipi kuhusu ndugu
yako, Aroni Mlawi? Ninajua yeye anaweza
kuzungumza vizuri. Naye yuko tayari njiani
kukulaki, na moyo wake utafurahi wakati
atakapokuona. 15 [j]Utazungumza naye
na kuweka maneno kinywani mwake.
Nitawasaidia ninyi wawili kusema, nami
nitawafundisha jambo la kufanya. 16 [k]Aroni
ataongea na watu badala yako na itakuwa
kwamba yeye amekuwa kinywa chako nawe
utakuwa kama Mungu kwake. 17 [l]Lakini
chukua fimbo hii mkononi mwako ili uweze
kuitumia kufanya ishara hizo za ajabu.”

*Mose Anarudi Misri*

18 Kisha Mose akarudi kwa Yethro
mkwewe akamwambia, “Niruhusu nirudi
kwa watu wangu Misri kuona kama yuko
hata mmoja wao ambaye bado anaishi.”
Yethro akamwambia, “Nenda, nami
nakutakia mema.”
19 [m]Basi BWANA alikuwa amemwambia
Mose huko Midiani, “Rudi Misri kwa
maana watu wote waliotaka kukuua
wamekufa.” 20 [n]Basi Mose akamchukua
mkewe na wanawe, akawapandisha juu ya
punda na kuanza safari kurudi Misri. Naye
akaichukua ile fimbo ya Mungu mkononi
mwake.
21 [o]BWANA akamwambia Mose,
“Utakaporudi Misri, hakikisha kwamba
utafanya mbele ya Farao maajabu yote
niliyokupa uwezo wa kuyafanya. Lakini
nitafanya moyo wake kuwa mgumu ili
kwamba asiwaruhusu watu waende.
22 [p]Kisha mwambie Farao, ‘Hili ndilo
asemalo BWANA: Israeli ni mwanangu

[a]**4:6** Law 13:2, 11; Hes 12:10; Kum 24:9; 2Fal 5:1; 2Nya 26:21
[b]**4:7** 2Fal 5:14; Mt 8:3; Lk 17:12-14
[c]**4:8** Kut 3:8; Amu 6:17; 1Fal 3:3; Isa 7:14; Yer 44:28-29
[d]**4:9** Kut 7:17-21
[e]**4:10** Kut 3:11
[f]**4:11** Kut 3:11; Lk 1:20, 64; Za 94:9; Mt 11:5; Yn 10:21
[g]**4:12** Kut 3:10; Hes 23:5; Kum 18:15-18; Isa 50:4; 51:16; Mt 10:19-20; Mk 13:11; Lk 12:12
[h]**4:13** Yon 1:1-3
[i]**4:14** Hes 11:1; 12:9; 16:15; 22:22; 24:10; 32:13; Kum 7:25; Ay 17:8; Yos 7:1; 1Sam 10:2-5
[j]**4:15** Hes 23:5, 12-16; Kum 18:18; Isa 51:16; 59:21; Yer 1:9; 31:33
[k]**4:16** Kut 7:1-2; Yer 15:19; 36:6; Hes 33:1; Za 77:20; 105:26; Mik 6:4
[l]**4:17** Kut 7:9-21; 8:5; 9:22; 10:12-15, 21-23; 14:15-26; 17:6; Hes 14:11; Kum 4:34; Za 74:9; 78:43; 105:27
[m]**4:19** Kut 2:15, 23; Mt 2:20
[n]**4:20** Kut 2:22; 18:3; Mdo 7:29
[o]**4:21** Kut 3:19, 20; 7:3, 13; 8:15, 32; 9:12, 17, 35; 10:20-27; 11:10; 14:4, 8; Kum 2:30; Yos 11:20; Za 105:25; Isa 6:10; 63:17; Yn 12:40; Rum 9:18
[p]**4:22** Mwa 10:15; Kum 32:6; Isa 9:6; 63:16; 64:8; Yer 3:19; 31:9; Hos 11:1; Mal 2:10; Rum 9:4; 2Kor 6:18

mzaliwa wa kwanza, 23 [a]nami nilikuambia,
“Ruhusu mwanangu aondoke, ili aweze
kuniabudu mimi.” Lakini ukakataa
kumruhusu kwenda, basi nitaua mwana
wako mzaliwa wa kwanza.’ ”
24 [b]Mose alipokuwa mahali pa kulala
wageni akiwa njiani kurudi Misri, BWANA
akakutana naye, akataka kumuua. 25 [c]Lakini
Sipora akachukua jiwe gumu, akakata govi
la mwanawe na kugusa nalo miguu ya
Mose. Sipora akasema, “Hakika wewe ni
bwana arusi wa damu kwangu.” 26 Sipora
alipomwita Mose, “Bwana arusi wa damu,”
alikuwa anamaanisha ile tohara. Baada ya
hayo BWANA akamwacha.
27 [d]BWANA akamwambia Aroni, “Nenda
jangwani ukamlaki Mose.” Basi akakutana
na Mose kwenye mlima wa Mungu,
akambusu. 28 Kisha Mose akamwambia
Aroni kila kitu BWANA alichomtuma
kusema, vilevile habari za ishara na
maajabu alizokuwa amemwamuru kufanya.
29 [e]Mose na Aroni wakawakusanya
wazee wote wa Waisraeli, 30 naye Aroni
akawaambia kila kitu BWANA alichokuwa
amemwambia Mose. Pia akafanya ishara
mbele ya watu, 31 [f]nao wakaamini. Nao
waliposikia kuwa BWANA anajishughulisha
nao, na kwamba ameona mateso yao,
walisujudu na kuabudu.

*Matofali Bila Nyasi*

5 [g]Baadaye Mose na Aroni wakaenda
kwa Farao, wakamwambia, “Hili ndilo
asemalo BWANA, Mungu wa Israeli:
‘Waruhusu watu wangu waende, ili waweze
kunifanyia sikukuu huko jangwani.’ ”
2 [h]Farao akasema, “Huyo BWANA ni nani,
hata nimtii na kuruhusu Israeli uende?
Simjui huyo BWANA wala sitawaruhusu
Israeli waende.”
3 [i]Ndipo Mose na Aroni wakasema,
“Mungu wa Waebrania amekutana nasi.
Sasa turuhusu tuwe na safari ya siku tatu
ya jangwani ili tukamtolee BWANA Mungu
wetu dhabihu, la sivyo aweza kutupiga sisi
kwa tauni au kwa upanga.”
4 [j]Lakini mfalme wa Misri akasema,
“Mbona ninyi Mose na Aroni mnawachukua
watu waache kazi zao? Rudini kwenye kazi
zenu!” 5 [k]Kisha Farao akasema, “Tazama,
sasa watu hawa ni wengi, nanyi mnawazuia
kufanya kazi.”
6 [l]Siku iyo hiyo Farao akatoa amri hii kwa
viongozi wa watumwa na wasimamizi wa
watu akawaambia: 7 [m]“Tangu sasa msiwape
hawa watu nyasi za kutengenezea matofali.
Wao wakusanye nyasi zao wenyewe.
8 [n]Lakini watakeni kutengeneza matofali
kiasi kile kile cha mwanzo, kiwango
kisipunguzwe. Wao ni wavivu, ndiyo
sababu wanalia, wakisema, ‘Turuhusiwe
twende kumtolea Mungu wetu dhabihu.’
9 Fanyeni kazi kuwa ngumu zaidi kwa
watu hao ili kwamba wakazane na kazi na
kuacha kusikiliza uongo.”
10 Basi viongozi wa watumwa na
wasimamizi wakaenda kuwaambia watu,
“Hivi ndivyo Farao asemavyo: ‘Sitawapa
tena nyasi. 11 Nendeni mkatafute nyasi
wenyewe popote mnapoweza kuzipata,
lakini kazi yenu haitapunguzwa hata
kidogo.’ ” 12 Basi watu wakatawanyika kote
nchini Misri kukusanya mabua ya kutumia
badala ya nyasi. 13 Viongozi wa watumwa
wakasisitiza, wakisema, “Timizeni kazi
mnayotakiwa kwa kila siku, kama wakati ule
mlipokuwa mkipewa nyasi.” 14 [o]Wasimamizi
wa Kiisraeli waliochaguliwa na viongozi wa
watumwa wa Farao walipigwa na kuulizwa,
“Kwa nini hamkutimiza kiwango chenu cha

---

[a]**4:23** Kut 3:18; 5:1; 7:16; 11:5; 12:12, 29; Mwa 49:3; Hes 8:17; 33:4; Za 78:51; 105:36; 135:8; 136:10
[b]**4:24** Hes 22:22
[c]**4:25** Kut 2:21; Mwa 17:14; Yos 5:2-3
[d]**4:27** Kut 3:1; Mwa 27:27; 29:13
[e]**4:29** Kut 3:16
[f]**4:31** Kut 2:25; 3:18; Mwa 16:11; 24:26
[g]**5:1** Kut 3:18; 4:23
[h]**5:2** Amu 2:10; Ay 21:15; Mal 3:14; Kut 3:19
[i]**5:3** Mwa 30:36; Law 26:25; Hes 14:12; Kum 28:21; 2Sam 24:13
[j]**5:4** Kut 1:11; 6:6-7
[k]**5:5** Mwa 12:2
[l]**5:6** Mwa 15:13
[m]**5:7** Mwa 11:3
[n]**5:8** Kut 10:11
[o]**5:14** Isa 10:24

kutengeneza matofali jana na leo, kama
mwanzoni?”
15 Ndipo wasimamizi wa Kiisraeli
wakaenda kumlilia Farao, wakisema:
“Mbona umewatendea watumishi wako
hivi? 16 Watumishi wako hawapewi nyasi,
hata hivyo tumeambiwa, ‘Tengenezeni
matofali!’ Watumishi wako wanapigwa,
lakini kosa ni la watu wako wenyewe.”
17 Farao akasema, “Ninyi ni wavivu
ndiyo sababu mnasema, ‘Turuhusu twende
tukamtolee BWANA dhabihu.’ 18 [a]Sasa
nendeni kazini. Hamtapewa nyasi zozote,
nanyi ni lazima mtengeneze matofali.”
19 Wasimamizi wa Kiisraeli walitambua
kuwa wako taabani walipoambiwa,
“Hamtakiwi kupunguza idadi ya matofali
mliotakiwa kutengeneza kila siku.”
20 Walipoondoka kwa Farao, wakawakuta
Mose na Aroni wakingojea kukutana
nao, 21 [b]wakawaambia Mose na Aroni,
“BWANA na awaangalie awahukumu ninyi!
Mmetufanya tunuke kwa Farao na maafisa
wake, nanyi mmeweka upanga mikononi
mwao ili kutuua sisi.”

*Mungu Anaahidi Ukombozi*

22 [c]Mose akarudi kwa BWANA na
kumwambia, “Ee Bwana, mbona
umewaletea watu hawa taabu? Kwa
nini basi ukanituma mimi? 23 [d]Tangu
nilipomwendea Farao kuzungumza naye
kwa jina lako, amewaletea taabu watu
hawa, nawe kamwe hujawakomboa watu
wako.”
6 [e]Kisha BWANA akamwambia Mose, “Sasa
utaona kitu nitakachomfanyia Farao:
Kwa sababu ya mkono wangu wenye nguvu
atawaachia watu waende; kwa sababu ya
mkono wangu wenye nguvu atawafukuza
waondoke nchini mwake.”
2 [f]Pia Mungu akamwambia Mose, “Mimi
ndimi BWANA. 3 [g]Nilimtokea Abrahamu,
Isaki na Yakobo kama Mungu Mwenyezi,[h]
ingawa sikuwajulisha Jina langu, Yehova,
Mimi mwenyewe sikujitambulisha kwao.
4 [i]Pia niliweka Agano langu nao kuwapa nchi
ya Kanaani, ambako waliishi kama wageni.
5 [j]Zaidi ya hayo, nimesikia kilio cha huzuni
cha Waisraeli ambao Wamisri wamewatia
utumwani, nami nimelikumbuka Agano
langu.
6 [k]“Kwa hiyo, waambie Waisraeli: ‘Mimi
ndimi BWANA, nami nitawatoa mtoke
katika kongwa la Wamisri. Nitawaweka
huru mtoke kuwa watumwa wao, nami
nitawakomboa kwa mkono ulionyooshwa
pamoja na matendo makuu ya hukumu.
7 [l]Nitawatwaa mwe watu wangu mwenyewe,
nami nitakuwa Mungu wenu. Ndipo mtajua
kuwa mimi ndimi BWANA Mungu wenu,
niliyewatoa chini ya kongwa la Wamisri.
8 [m]Nami nitawaleta mpaka nchi niliyoapa
kwa mkono ulioinuliwa kumpa Abrahamu,
Isaki na Yakobo. Nitawapa iwe milki yenu.
Mimi ndimi BWANA.’ ”
9 [n]Mose akawaarifu Waisraeli jambo
hili, lakini hawakumsikiliza kwa sababu

[a]**5:18** Mwa 15:13
[b]**5:21** Mwa 34:30; 16:5; Kut 1:13; 14:11; 16:3; Hes 14:3; 20:3
[c]**5:22** Kut 1:12; Yos 7:7; Hes 11:11
[d]**5:23** Yer 4:10; 20:7; Eze 14:9
[e]**6:1** Kut 3:20; 11:1; 12:31-39; Kum 5:15
[f]**6:2** Kut 3:14-15; 7:5; 8:22; 10:2; 12:12; 14:4, 18; 16:12; Law 11:44; 18:21; 20:7; Isa 41:20; 43:11; 49:23; 60:16; Eze 13:9; 25:17; 36:38; 37:6, 13; Yoe 2:27
[g]**6:3** Mwa 7:1; 2Sam 7:26; Za 48:10; 61:5; 68:4; 83:18; 99:3; Isa 52:6; Kut 3:14, 15; Yn 8:58
[h]3 Mungu Mwenyezi hapa ni jina la Kiebrania, El-Shaddai (yaani Mungu Mwenye utoshelevu wote).
[i]**6:4** Mwa 6:18; 12:7; 15:18; 17:8; Mdo 7:5; Rum 4:13; Gal 3:16; Ebr 11:8-10
[j]**6:5** Kut 2:23; Mdo 7:34; Mwa 9:15
[k]**6:6** Kut 3:8, 19-20; 12:17, 51; 15:13; 16:6; 20:2; 29:46; Law 22:33; 26:13; Kum 6:12; 7:8; 9:26; Za 9:16; 19:14; 34:22; 74:2; 77:15; 81:10; 105:27; 136:11; Yer 2:6; 15:21; 31:11; 50:34; Hos 13:4; Amo 2:10; Mik 6:4; 1Nya 17:21; Isa 29:22; 35:9; 44:23; 48:20; Mdo 13:17
[l]**6:7** Mwa 17:7; Kut 34:9; Eze 11:19-20; 39:6; Rum 9:4; 1Fal 20:13, 28; Isa 43:10; Yoe 3:17
[m]**6:8** Mwa 12:7; 14:22; Kut 3:8; Yer 11:5; Eze 20:6; Ufu 10:5-6; Za 136:21-22; Law 18:21
[n]**6:9** Mwa 34:30; Kut 2:23

ya maumivu makuu ya moyoni na utumwa
wa kikatili.
10 Ndipo Bwana akamwambia Mose,
11 [a]“Nenda, mwambie Farao mfalme wa
Misri awaachie Waisraeli waondoke nchini
mwake.”
12 [b]Lakini Mose akamwambia Bwana,
“Ikiwa Waisraeli hawatanisikiliza, kwa
nini yeye Farao anisikilize mimi, ambaye
huzungumza kwa kigugumizi?”

*Orodha Ya Jamaa Ya Mose Na Aroni*

13 [c]Ndipo Bwana akanena na Mose na
Aroni kuhusu Waisraeli na Farao mfalme
wa Misri, naye akawaamuru wawatoe
Waisraeli kutoka Misri.

14 [d]Hawa walikuwa wakuu wa jamaa
zao:

Wana wa Reubeni mzaliwa wa
kwanza wa kiume wa Israeli walikuwa
Hanoki, Palu, Hesroni na Karmi. Hawa
walikuwa ndio koo za Reubeni.
15 [e]Wana wa Simeoni walikuwa
Yemueli, Yamini, Ohadi, Yakini, Sohari
na Shauli mwana wa mwanamke
Mkanaani. Hawa walikuwa ndio koo
za Simeoni.
16 [f]Haya ndiyo majina ya wana
wa Lawi kufuatana na orodha zao:
Gershoni, Kohathi na Merari. Lawi
aliishi miaka 137.
17 [g]Wana wa Gershoni kwa koo,
walikuwa Libni na Shimei.
18 [h]Wana wa Kohathi walikuwa
Amramu, Ishari, Hebroni na Uzieli.
Kohathi aliishi miaka 133.
19 [i]Wana wa Merari walikuwa Mahli
na Mushi.

Hizi ndizo zilizokuwa koo za Lawi
kufuatana na orodha zao.
20 [j]Amramu akamwoa Yokebedi,
shangazi yake, ambaye alimzalia Aroni
na Mose. Amramu aliishi miaka 137.
21 [k]Wana wa Ishari walikuwa Kora,
Nefegi na Zikri.
22 [l]Wana wa Uzieli walikuwa
Mishaeli, Elisafani na Sithri.
23 [m]Aroni akamwoa Elisheba binti wa
Aminadabu ndugu yake Nashoni, naye
akamzalia Nadabu, Abihu, Eleazari na
Ithamari.
24 [n]Wana wa Kora walikuwa Asiri,
Elikana na Abiasafu. Hawa walikuwa
ndio koo za Kora.
25 [o]Eleazari mwana wa Aroni
akamwoa mmoja wa binti za Putieli,
naye akamzalia Finehasi.

Hawa walikuwa ndio wakuu wa
jamaa za Walawi, ukoo kwa ukoo.

26 [p]Hawa walikuwa Aroni na Mose wale
wale ambao Bwana aliwaambia, “Watoeni
Waisraeli katika nchi ya Misri kwa vikosi
vyao.” 27 Ndio hao hao waliozungumza na
Farao mfalme wa Misri kuhusu kuwatoa
Waisraeli Misri. Ilikuwa ni huyo Mose na
huyo Aroni.

*Aroni Kuzungumza Badala Ya Mose*

28 Bwana aliponena na Mose huko Misri,
29 akamwambia, “Mimi ndimi Bwana.
Mwambie Farao mfalme wa Misri kila kitu
nikuambiacho.”
30 [q]Lakini Mose akamwambia Bwana,
“Kwa kuwa mimi huzungumza kwa
kigugumizi, Farao atanisikiliza mimi?”
7 [r]Kisha Bwana akamwambia Mose,
“Tazama, nimekufanya kuwa kama

[a]**6:11** Kut 3:18
[b]**6:12** Kut 3:18; 4:10
[c]**6:13** Kut 3:10
[d]**6:14** Kut 13:3; Hes 1:1; 26:4; Mwa 29:32
[e]**6:15** Mwa 29:33
[f]**6:16** Mwa 29:34; 46:11; Hes 3:17; Yos 21:7; 1Nya 6:1, 16
[g]**6:17** Hes 3:18; 1Nya 6:17
[h]**6:18** Hes 3:19, 27; 1Nya 6:18; 23:12
[i]**6:19** 1Nya 6:19; 23:21; Hes 3:20, 33
[j]**6:20** Kut 2:1-2; 1Nya 23:13; Hes 26:59
[k]**6:21** 1Nya 6:38
[l]**6:22** Law 10:4; Hes 3:30; 2Nya 29:13
[m]**6:23** Rut 4:19-20; 1Nya 2:10; 6:3; 24:1; Hes 2:3; 3:2, 32; 4:28; 16:37-39; 26:60; Kum 10:6; Kut 24:1; Law 10:1-6; 10:12-16
[n]**6:24** Hes 16:1; 1Nya 6:22, 37
[o]**6:25** Hes 25:7; 31:6; Yos 24:33; Za 106:30
[p]**6:26** Kut 3:10; 7:4; 12:17, 41, 51
[q]**6:30** Kut 3:11
[r]**7:1** Kut 4:15, 16; Mdo 14:12

Mungu kwa Farao, naye Aroni, huyo ndugu
yako, atakuwa nabii wako. 2 Utasema
kila kitu nitakachokuagiza, naye Aroni
ndugu yako atamwambia Farao awaachie
Waisraeli watoke katika nchi yake. 3 [a]Lakini
nitaufanya moyo wa Farao kuwa mgumu.
Ingawa nitazidisha ishara na maajabu
katika Misri, 4 [b]hatawasikiliza. Kisha
nitaupeleka mkono wangu juu ya Misri, na
kwa matendo makuu ya hukumu nitavitoa
vikundi vyangu, watu wangu Waisraeli.
5 [c]Nao Wamisri watajua kuwa Mimi ndimi
BWANA nitakapounyoosha mkono wangu
dhidi ya Misri na kuwatoa Waisraeli watoke
humo."
6 [d]Mose na Aroni wakafanya sawasawa
kama vile BWANA alivyowaagiza. 7 [e]Mose
alikuwa na umri wa miaka themanini na
Aroni alikuwa na umri wa miaka themanini
na mitatu walipozungumza na Farao.

### *Fimbo Ya Aroni Yawa Nyoka*

8 BWANA akamwambia Mose na Aroni,
9 [f]"Farao atakapowaambia, 'Fanyeni
muujiza,' basi mwambie Aroni, 'Chukua
fimbo yako na uitupe chini mbele ya Farao,'
nayo fimbo itakuwa nyoka."
10 Ndipo Mose na Aroni wakaenda kwa
Farao wakafanya sawasawa kama vile
BWANA alivyoagiza. Aroni akaitupa ile
fimbo yake chini mbele ya Farao na maafisa
wake, nayo ikawa nyoka. 11 [g]Farao naye
akawaita watu wenye maarifa na wachawi
na waganga wa Kimisri, nao wakafanya
vivyo hivyo kwa siri ya uganga wao. 12 Kila
mmoja alitupa fimbo yake chini, nayo ikawa
nyoka. Lakini fimbo ya Aroni ikazimeza zile
fimbo zao. 13 [h]Hata hivyo moyo wa Farao
ukawa mgumu, naye hakuwasikiliza Mose
na Aroni, sawasawa kama vile BWANA
alivyokuwa amesema.

### *Pigo La Kwanza: Damu*

14 [i]Kisha BWANA akamwambia Mose,
"Moyo wa Farao ni mgumu, anakataa
kuwaachia watu kuondoka. 15 Nenda
kwa Farao asubuhi wakati anapokwenda
mtoni. Ngoja ukingoni mwa Naili ili
uonane naye, na uchukue mkononi mwako
fimbo ile iliyobadilishwa kuwa nyoka.
16 [j]Kisha umwambie, 'BWANA, Mungu
wa Waebrania, amenituma nikuambie:
Waachie watu wangu waende, ili wapate
kuniabudu jangwani. Lakini hadi sasa
hujasikiliza. 17 [k]Hili ndilo BWANA asemalo:
Kwa hili utajua kuwa Mimi ndimi BWANA:
Fimbo iliyo mkononi mwangu nitapiga
nayo maji ya Naili nayo yatabadilika kuwa
damu. 18 [l]Samaki waliomo katika Mto Naili
watakufa, nao mto utanuka vibaya, Wamisri
hawataweza kunywa hayo maji yake.' "
19 [m]BWANA akamwambia Mose,
"Mwambie Aroni, 'Chukua ile fimbo yako
unyooshe mkono wako juu ya maji ya
Misri, juu ya chemchemi na mifereji, juu
ya madimbwi na mabwawa yote,' navyo
vitabadilika kuwa damu. Damu itakuwa
kila mahali katika Misri, hata kwenye
vyombo vya miti na vya mawe."
20 [n]Mose na Aroni wakafanya kama vile
BWANA alivyokuwa amewaagiza. Akainua
fimbo yake machoni pa Farao na maafisa
wake na kuyapiga maji ya Mto Naili,
na maji yote yakabadilika kuwa damu.
21 Samaki katika Mto Naili wakafa, nao
mto ukanuka vibaya sana kiasi kwamba
Wamisri hawakuweza kunywa maji yake.
Damu ilikuwa kila mahali katika nchi ya
Misri.

[a]**7:3** Kut 3:20; 4:21; Rum 9:18; Mdo 7:36
[b]**7:4** Kut 3:20; 6:26; 8:15-19; 9:12; 11:9; Mdo 7:36
[c]**7:5** Kut 3:20; 6:2; Za 138:7; Eze 6:14; 25:13
[d]**7:6** Mwa 6:22
[e]**7:7** Kum 31:2; 34:7; Mdo 7:23-30
[f]**7:9** Kum 6:22; 2Fal 19:29; Za 78:43; 105:27; Isa 7:11; 37:30; 38:7-8; 55:13; Yn 2:11; Kut 4:2-5
[g]**7:11** Kut 22:18; Kum 18:10; 1Sam 6:12; 2Fal 21:6; Isa 2:6; 47:12; Yer 27:9; Mal 3:5; Mwa 41:8; 2Tim 3:8; Mt 24:24
[h]**7:13** Kut 4:21
[i]**7:14** Kut 7:22; 9:7; 10:20-27; 8:15, 32
[j]**7:16** Kut 3:18
[k]**7:17** Kut 4:9; 6:2; 14:25; Ufu 11:6; 16:4
[l]**7:18** Isa 19:6; Za 78:44
[m]**7:19** Kut 4:2; 14:21; 2Fal 5:11
[n]**7:20** Kut 17:5; Za 78:44; 105:29; 114:3; Hab 3:8

22 [a]Lakini waganga wa Misri kwa kutumia
siri ya uganga wao wakafanya vivyo
hivyo, nao moyo wa Farao ukawa mgumu,
hakuwasikiliza Mose na Aroni, kama vile
BWANA alivyokuwa amesema. 23 Badala
yake, Farao akageuka, akaenda kwenye
jumba lake la kifalme, wala hakulitia hili
moyoni. 24 Nao Wamisri wote wakachimba
kandokando ya Mto Naili kupata maji ya
kunywa, kwa sababu hawakuweza kunywa
maji ya mto.

*Pigo La Pili: Vyura*

25 Zilipita siku saba baada ya BWANA
kuyapiga maji ya Mto Naili.

8 [b]Ndipo BWANA akamwambia Mose,
"Nenda kwa Farao ukamwambie, 'Hili
ndilo asemalo BWANA: Waachie watu
wangu waende, ili wapate kuniabudu.
2 [c]Kama ukikataa kuwaruhusu kuondoka,
basi nitaipiga nchi yako yote kwa kuwaletea
vyura. 3 [d]Mto Naili utafurika vyura. Watakuja
kwenye jumba lako la kifalme na katika
chumba chako cha kulala na kitandani
mwako, katika nyumba za maafisa wako
na kwa watu wako, vyura hao wataingia
katika meko yenu na kwenye vyombo vya
kukandia unga. 4 Vyura watapanda juu
yako, juu ya watu wako na maafisa wako
wote.' "

5 [e]Ndipo BWANA akamwambia Mose,
"Mwambie Aroni, 'Nyoosha mkono wako
ukiwa na ile fimbo yako juu ya vijito,
mifereji na madimbwi, fanya vyura waje
juu ya nchi ya Misri.' "

6 [f]Ndipo Aroni akaunyoosha mkono wake
juu ya maji ya Misri, nao vyura wakatokea
na kuifunika nchi. 7 [g]Lakini waganga
wakafanya vivyo hivyo kwa siri ya uganga
wao, nao pia wakafanya vyura kuja juu ya
nchi ya Misri.

8 [h]Ndipo Farao akamwita Mose na Aroni
na kusema, "Mwombeni BWANA awaondoe
vyura kutoka kwangu na kwa watu wangu,
nami nitawaachia watu wenu waende
kumtolea BWANA dhabihu."

9 [i]Mose akamwambia Farao, "Ninakupa
heshima ya kuamua ni wakati gani wa
kukuombea wewe, maafisa wako na watu
wako ili kwamba vyura watoke kwenu na
kwenye nyumba zenu. Isipokuwa wale
walio katika Mto Naili."

10 [j]Farao akasema, "Kesho."

Mose akamjibu, "Itakuwa kama
unavyosema, ili upate kujua kwamba
hakuna yeyote kama BWANA Mungu wetu.
11 Vyura wataondoka kwako na katika
nyumba zako, kwa maafisa wako na kwa
watu wako, ila watabakia katika Mto Naili
tu."

12 Baada ya Mose na Aroni kuondoka
kwa Farao, Mose akamlilia BWANA
kuhusu vyura aliokuwa amewaleta kwa
Farao. 13 [k]Naye BWANA akafanya lile
Mose alilomwomba. Vyura wakafia ndani
ya nyumba, viwanjani na mashambani.
14 Wakayakusanya malundo, nchi nzima
ikanuka. 15 [l]Lakini Farao alipoona
pametokea nafuu, akaushupaza moyo wake
na hakuwasikiliza Mose na Aroni, kama vile
BWANA alivyokuwa amesema.

*Pigo La Tatu: Viroboto*

16 [m]Ndipo BWANA akamwambia Mose,
"Mwambie Aroni, 'Nyoosha fimbo yako
uyapige mavumbi ya ardhi,' nayo nchi
yote ya Misri mavumbi yatakuwa viroboto."
17 [n]Wakafanya hivyo, Aroni aliponyoosha
mkono wake wenye fimbo na kuyapiga
mavumbi ya nchi, viroboto wakawajia watu

---

[a]**7:22** Mwa 41:8; Mt 24:24; Kut 8:19; Za 105:28
[b]**8:1** Kut 3:12; 4:23; 5:1; 9:1
[c]**8:2** Za 78:45; 105:30; Ufu 16:13
[d]**8:3** Kut 10:6; 12:34
[e]**8:5** Kut 4:2, 17; 7:9-23; 10:13, 21-22; 14:27
[f]**8:6** Za 78:45; 105:30
[g]**8:7** Kut 7:11; Mt 24:24
[h]**8:8** Kut 9:28; 10:8, 17; Hes 21:7; 1Sam 12:19; 1Fal 13:6; Yer 42:2; Mdo 8:24
[i]**8:9** Kut 9:5
[j]**8:10** Kut 9:14; 15:11; Kum 3:24; 4:35; 33:26; 2Sam 7:22; 1Fal 8:23; 1Nya 17:20; 2Nya 6:14; Za 71:19; 86:8; 89:6; Isa 40:18; 42:8; 46:9; Yer 49:19; Mik 7:18
[k]**8:13** Yak 5:16-18
[l]**8:15** Mhu 8:11; Kut 7:14
[m]**8:16** Kut 4:2
[n]**8:17** Za 105:31

na wanyama. Mavumbi yote katika nchi ya
Misri yakawa viroboto. 18 [a]Lakini waganga
walipojaribu kutengeneza viroboto kwa siri
ya uganga wao, hawakuweza. Nao viroboto
walikuwa juu ya watu na wanyama.
19 [b]Waganga wale wakamwambia Farao,
“Hiki ni kidole cha Mungu.” Lakini moyo wa
Farao ukawa mgumu naye hakuwasikiliza,
kama vile Bwana alivyosema.

*Pigo La Nne: Mainzi*

20 [c]Kisha Bwana akamwambia Mose,
“Amka mapema asubuhi na usimame mbele
ya Farao wakati anapokwenda mtoni nawe
umwambie, ‘Hili ndilo Bwana asemalo:
Waachie watu wangu waende, ili wapate
kuniabudu. 21 Kama hutawaachia watu
wangu waondoke nitakupelekea makundi
ya mainzi juu yako, kwa maafisa wako,
kwa watu wako na kwenye nyumba zenu.
Nyumba za Wamisri zitajazwa mainzi, hata
na ardhi yote ya Misri.
22 [d]“ ‘Lakini siku ile nitafanya kitu tofauti
katika nchi ya Gosheni, ambapo watu wangu
wanaishi, hapatakuwepo na makundi ya
mainzi, ili mpate kujua kwamba Mimi,
Bwana, niko katika nchi hii. 23 [e]Nitaweka
tofauti kati ya watu wangu na watu wenu.
Ishara hii ya ajabu itatokea kesho.’ ”
24 [f]Naye Bwana akafanya hivyo. Makundi
makubwa ya mainzi yalimiminika katika
jumba la kifalme la Farao na katika nyumba
za maafisa wake, pia nchi yote ya Misri
ikaharibiwa na mainzi.
25 [g]Ndipo Farao akamwita Mose na Aroni
na kuwaambia, “Nendeni mkamtolee
Mungu wenu dhabihu katika nchi hii.”
26 [h]Lakini Mose akamwambia, “Hilo
halitakuwa sawa. Dhabihu tutakazomtolea
Bwana Mungu wetu zitakuwa chukizo kwa
Wamisri. Kama tukitoa dhabihu ambazo ni
chukizo mbele yao, je, hawatatupiga mawe?
27 [i]Ni lazima twende mwendo wa siku tatu
mpaka tufike jangwani ili tumtolee Bwana
Mungu wetu dhabihu, kama alivyotuagiza.”
28 [j]Farao akamwambia, “Nitawaruhusu
mwende kumtolea Bwana Mungu
wenu dhabihu huko jangwani, lakini
hamna ruhusa kwenda mbali sana. Sasa
mniombee.”
29 [k]Mose akajibu, “Mara tu
nitakapoondoka, nitamwomba Bwana
na kesho mainzi yataondoka kwa Farao,
kwa maafisa wake na kwa watu wake.
Hakikisha tu kwamba Farao hatatenda kwa
udanganyifu tena kwa kutokuwaachia watu
waende kumtolea Bwana dhabihu.”
30 [l]Ndipo Mose akamwacha Farao na
kumwomba Bwana, 31 naye Bwana
akafanya lile Mose alilomwomba. Mainzi
yakaondoka kwa Farao, kwa maafisa
wake na kwa watu wake, wala hakuna
hata inzi aliyebakia. 32 [m]Lakini wakati huu
pia Farao akaushupaza moyo wake, wala
hakuwaruhusu Waisraeli waondoke.

*Pigo La Tano: Vifo Vya Mifugo*

9 [n]Ndipo Bwana akamwambia Mose,
“Nenda kwa Farao ukamwambie, ‘Hili
ndilo Bwana, Mungu wa Waebrania
asemalo: “Waachie watu wangu waende
ili wapate kuniabudu.” 2 Kama ukikataa
kuwaachia waende, nawe ukiendelea
kuwashikilia, 3 [o]mkono wa Bwana
utaleta pigo baya kwa mifugo yako, juu
ya farasi wako, punda, ngamia, ng’ombe
wako, kondoo na mbuzi. 4 [p]Lakini Bwana
ataweka tofauti kati ya mifugo ya Israeli

---

[a]**8:18** Kut 7:11; 9:11; Dan 5:8
[b]**8:19** Kut 7:5, 13-15; 10:7; 12:33; 31:18; 1Sam 6:9; Neh 9:6; Za 8:3; 33:6; Lk 11:20
[c]**8:20** Kut 7:15; 9:13; 3:18
[d]**8:22** Mwa 45:10; Kut 7:5; 9:4-6, 26, 29; 10:23; 11:7; 12:13; 19:5; Kum 4:20; 7:6; 14:2; 26:18; 1Fal 8:36; Ay 36:11; Za 33:12; 135:4; Mal 3:17
[e]**8:23** Kut 9:4-6; 10:23; 11:7; 12:23-27
[f]**8:24** Za 78:45; 105:31
[g]**8:25** Kut 9:27; 10:16; 12:31
[h]**8:26** Mwa 43:32
[i]**8:27** Mwa 30:36; Kut 3:18
[j]**8:28** Yer 37:3; Mdo 8:24
[k]**8:29** Kut 9:30; 10:11; Isa 26:10
[l]**8:30** Kut 9:33; 10:18
[m]**8:32** Kut 7:14
[n]**9:1** Kut 8:1
[o]**9:3** Kut 7:4; 1Sam 5:6; Ay 13:21; Za 32:4; 39:10; 78:50; Mdo 13:11; Law 26:25; Amo 4:10
[p]**9:4** Kut 8:23

na ile ya Misri, kwamba hakuna mnyama
wa Mwisraeli atakayekufa.' "
5 BWANA akaweka wakati na kusema,
"Kesho BWANA atalitenda hili katika
nchi." 6 [a]Siku iliyofuata BWANA akalitenda:
Mifugo yote ya Wamisri ikafa, lakini
hakuna hata mnyama mmoja wa wana
wa Israeli aliyekufa. 7 [b]Farao akatuma
watu kuchunguza, nao wakakuta
kuwa hakuna hata mnyama mmoja wa
Waisraeli aliyekufa. Lakini moyo wa Farao
haukukubali kuwaachia watu waende.

*Pigo La Sita: Majipu*

8 Kisha BWANA akamwambia Mose na
Aroni, "Chukueni majivu ya tanuru, naye
Mose ayarushe angani mbele ya Farao.
9 [c]Yatakuwa vumbi jepesi juu ya nchi yote
ya Misri, pia yatatokea majipu yenye kufura
juu ya watu na wanyama katika nchi yote."
10 Basi wakachukua majivu kwenye
tanuru na kusimama mbele ya Farao.
Mose akayarusha hewani, nayo majipu
yenye kufura yakatokea miilini mwa watu
na wanyama. 11 [d]Waganga hawakuweza
kusimama mbele ya Mose kwa sababu ya
majipu yale yaliyokuwa miilini mwao na
juu ya miili ya Wamisri wote. 12 [e]Lakini
BWANA akaufanya moyo wa Farao kuwa
mgumu, naye hakuwasikiliza Mose na
Aroni, sawasawa kama vile BWANA
alivyokuwa amemwambia Mose.

*Pigo La Saba: Mvua Ya Mawe*

13 [f]Kisha BWANA akamwambia Mose,
"Amka mapema asubuhi, usimame mbele
ya Farao, umwambie, 'Hili ndilo asemalo
BWANA, Mungu wa Waebrania: Waachie
watu wangu waende, ili kwamba waweze
kuniabudu, 14 [g]au wakati huu nitaleta
mapigo yangu yenye nguvu dhidi yako,
maafisa wako na watu wako, ili upate
kujua kuwa hakuna mwingine kama Mimi
katika dunia yote. 15 [h]Kwa kuwa mpaka sasa
ningelikuwa nimenyoosha mkono wangu
na kukupiga wewe na watu wako kwa pigo
ambalo lingekufutilia mbali juu ya nchi.
16 [i]Lakini nimekuinua wewe kwa kusudi
hili hasa, ili nipate kukuonyesha uwezo
wangu, na ili Jina langu lipate kutangazwa
duniani yote. 17 Bado unaendelea kujiinua
juu ya watu wangu, wala hutaki kuwaachia
waende. 18 [j]Kwa hiyo, kesho wakati kama
huu nitaleta mvua mbaya sana ya mawe
ambayo haijapata kunyesha katika nchi ya
Misri, tangu siku ilipoumbwa mpaka leo.
19 Sasa toa amri urudishe wanyama wote
watoke malishoni na chochote ambacho
kipo mashambani waje mpaka mahali
pa usalama, kwa sababu mvua ya mawe
itanyesha juu ya kila mtu na kila mnyama
ambaye hajaletwa ndani ambao bado wako
nje mashambani, nao watakufa.' "
20 [k]Wale maafisa wa Farao ambao
waliliogopa neno la BWANA wakafanya
haraka kuwaleta watumwa wao na mifugo
yao ndani. 21 [l]Lakini wale waliopuuza neno
la BWANA wakawaacha watumwa wao na
mifugo yao shambani.
22 Ndipo BWANA akamwambia Mose,
"Nyoosha mkono wako kuelekea angani
ili kwamba mvua ya mawe inyeshe juu ya
Misri yote, juu ya watu, wanyama na juu
ya kila kitu kiotacho katika mashamba
ya Misri." 23 [m]Mose alipoinyoosha fimbo
yake kuelekea angani, BWANA akatuma
ngurumo na mvua ya mawe, umeme wa
radi ulimulika hadi nchi. Kwa hiyo BWANA
akaifanya mvua ya mawe kunyesha juu ya
nchi ya Misri, 24 mvua ya mawe ikanyesha
na radi ikamulika pote. Ikawa dhoruba ya

---

[a]**9:6** Kut 11:5; 12:29; Za 78:48-50
[b]**9:7** Kut 7:14, 22; 8:32
[c]**9:9** Law 13:18-19; 2Fal 20:7; Ay 2:7; Isa 38:21; Ufu 16:2
[d]**9:11** Kut 8:18
[e]**9:12** Kut 4:21; 7:4
[f]**9:13** Kut 3:18
[g]**9:14** Kut 8:10; 15:11; 1Sam 2:2; 2Sam 7:22; 1Fal 8:23; 1Nya 17:20; Za 35:10; 71:19; 86:8; 89:6; Isa 46:9; Yer 10:6; Mik 7:18
[h]**9:15** Kut 3:20
[i]**9:16** Mit 16:4; Kut 14:4, 17, 31; Za 20:6; 25:11; 68:28; 71:18; 106:8; 109:21; Rum 9:17
[j]**9:18** Yos 10:11; Za 78:47-48; 105:32; 148:8; Isa 30:30; Eze 38:22; Hag 2:17; Kut 9:24; 10:6
[k]**9:20** Mit 13:13
[l]**9:21** Mwa 19:14; Eze 33:4-5
[m]**9:23** Kut 20:18; 1Sam 12:17; Za 18:13; 29:3; 68:33; 77:17; 104:7; Ufu 8:7; 16:21

kutisha ambayo haijakuwako katika nchi
ya Misri, tangu nchi hiyo iwe taifa. 25 [a]Mvua
ya mawe ikaharibu kila kitu katika nchi ya
Misri kilichokuwa katika mashamba, watu
na wanyama, ikaharibu kila kitu kinachoota
mashambani na kuvunja kila mti. 26 [b]Mahali
pekee ambapo mvua ya mawe haikunyesha
ni nchi ya Gosheni, ambako Waisraeli
waliishi.
27 [c]Ndipo Farao akawaita Mose na Aroni
akawaambia, “Wakati huu nimetenda
dhambi. BWANA ni mwenye haki, mimi
na watu wangu ni wakosaji. 28 [d]Mwombeni
BWANA, kwa kuwa tumepata ngurumo na
mvua za mawe za kututosha. Nitawaachia
mwondoke; hamtahitaji kungoja zaidi.”
29 [e]Mose akamjibu, “Nitakapokuwa
nimetoka nje ya mji, nitanyoosha mikono
yangu juu kumwomba BWANA. Ngurumo
zitakoma na hapatakuwepo mvua ya mawe
tena, ili upate kujua kuwa, nchi ni mali ya
BWANA. 30 [f]Lakini ninajua kuwa wewe na
maafisa wako bado hammwogopi BWANA
Mungu.”
31 [g](Kitani na shayiri viliharibiwa, kwa
kuwa shayiri ilikuwa na masuke, na
kitani ilikuwa katika kutoa maua. 32 [h]Hata
hivyo, ngano na jamii nyingine ya ngano
hazikuharibiwa kwa sababu zilikuwa
hazijakomaa bado.)
33 Kisha Mose akaondoka kwa Farao
akaenda nje ya mji. Mose akanyoosha
mikono yake kuelekea kwa BWANA,
ngurumo na mvua ya mawe vikakoma,
mvua haikuendelea tena kunyesha nchini.
34 Farao alipoona kwamba mvua ya mawe
na ngurumo zimekoma, akafanya dhambi
tena. Yeye na maafisa wake wakafanya
mioyo yao kuwa migumu. 35 [i]Kwa hiyo
moyo wa Farao ukawa mgumu, wala
hakuwaachia Waisraeli waende, kama vile
BWANA alivyokuwa amesema kupitia Mose.

*Pigo La Nane: Nzige*

10 [j]Ndipo BWANA akamwambia Mose,
“Nenda kwa Farao, kwa kuwa
nimeufanya moyo wake kuwa mgumu na
mioyo ya maafisa wake ili kwamba nipate
kutenda ishara hizi zangu za ajabu miongoni
mwao 2 [k]ili upate kuwaeleza watoto wako
na wajukuu wako jinsi nilivyowatendea
Wamisri kwa ukali na jinsi nilivyofanya
ishara zangu miongoni mwao, nanyi mpate
kujua kuwa Mimi ndimi BWANA.”
3 [l]Kwa hiyo Mose na Aroni wakaenda kwa
Farao na kumwambia, “Hili ndilo BWANA,
Mungu wa Waebrania, asemalo: ‘Utaendelea
hata lini kukataa kunyenyekea mbele yangu?
Waachie watu wangu waende, ili wapate
kuniabudu. 4 [m]Kama ukikataa kuwaachia
waende, kesho nitaleta nzige katika nchi
yako. 5 [n]Nao watafunika uso wa ardhi hata
usionekane. Watatafuna mabaki machache
yaliyobakizwa baada ya ile mvua ya mawe,
yaani pamoja na kila mti unaoota katika
mashamba yenu. 6 [o]Nzige hao watajaza
nyumba zako, za maafisa wako wote na
za Wamisri wote. Jambo ambalo baba zenu
wala babu zenu hawajapata kuona tangu
siku ile walipoanza kuishi katika nchi hii
mpaka leo hii.’ ” Ndipo Mose akageuka na
kumwacha Farao.

---

[a]**9:25** Za 105:32-33; Eze 13:13
[b]**9:26** Isa 32:18-20; Kut 10:23; 11:7; 12:13; Amo 4:7
[c]**9:27** Kut 10:16; Hes 14:40; Kum 1:41; Yos 7:11; Amu 10:10; 1Sam 15:24; 24:17; 26:21; Za 11:7; 116:5; 119:135; 129:4; 145:17; Yer 12:1; Mao 1:18
[d]**9:28** Kut 8:8; Mdo 8:24
[e]**9:29** 1Fal 8:22; Ay 11:13; Za 77:2; 88:9; 143:6; Isa 1:15; Kut 19:5; Ay 41:11; Za 24:1; 50:12; 1Kor 10:26
[f]**9:30** Kut 8:29
[g]**9:31** Kum 8:8; Rut 1:22; 2:23; 2Sam 14:30; 17:28; Isa 28:25; Eze 4:9
[h]**9:32** Isa 28:25
[i]**9:35** Kut 4:2
[j]**10:1** Kut 4:21; 3:19; 7:3; Yos 24:17; Neh 9:10; Za 74:9; 105:26-30
[k]**10:2** Kut 12:26-27; 13:8, 14; Kum 4:9; 6:20; 32:7; Yos 4:6; Za 71:18; 78:4-5; Kut 6:2
[l]**10:3** 1Fal 21:29; 2Fal 22:19; 2Nya 7:14; 12:7; 33:23; 34:27; Ay 42:6; Isa 58:3; Dan 5:22; Yak 4:10; 1Pet 5:6
[m]**10:4** Kut 8:2; 9:2; Kum 28:38; Za 105:34; Mit 30:27; Yoe 1:4; Ufu 9:3
[n]**10:5** Kut 9:32; Yoe 1:4
[o]**10:6** Yoe 2:9; Kut 9:18

7 [a]Maafisa wa Farao wakamwambia,
“Mpaka lini huyu mtu atakuwa tanzi kwetu?
Waachie hao watu waende zao, ili wapate
kumwabudu BWANA Mungu wao. Je, bado
hutambui kuwa Misri imeangamia?”
8 [b]Ndipo Mose na Aroni wakaletwa kwa
Farao. Farao akawaambia, “Nendeni,
mkamwabudu BWANA Mungu wenu. Lakini
ni nani hasa watakaokwenda?”
9 [c]Mose akajibu, “Tutakwenda na vijana
wetu na wazee, pamoja na wana wetu
na binti zetu, pia pamoja na kondoo
zetu, ng’ombe, mbuzi, farasi na punda
kwa sababu tutaadhimisha sikukuu kwa
BWANA.”
10 Farao akasema, “BWANA awe pamoja
nanyi, kama nikiwaruhusu mwondoke
pamoja na wanawake wenu na watoto
wenu! Ni wazi kwamba mna makusudi
mabaya. 11 La hasha! Wanaume peke yao
na waende, wakamwabudu BWANA, kwa
kuwa hilo ndilo mmekuwa mkiomba.” Kwa
hiyo Mose na Aroni wakaondolewa mbele
ya Farao.
12 [d]Basi BWANA akamwambia Mose,
“Nyoosha mkono wako juu ya Misri ili
kundi la nzige liweze kuingia juu ya nchi
na kutafuna kila kitu kiotacho katika
mashamba na kila kitu kilichosazwa na
ile mvua ya mawe.”
13 [e]Kwa hiyo Mose akanyoosha fimbo
yake juu ya Misri, BWANA akauleta upepo
wa mashariki ukavuma katika nchi yote
mchana wote na usiku kucha, kufikia
asubuhi upepo ukawa umeleta nzige.
14 [f]Wakaivamia Misri yote na kukaa kila
eneo la nchi kwa wingi. Kamwe hapajapata
kuwepo pigo la nzige kama hilo, wala
halitakuwepo tena. 15 [g]Wakafunika ardhi
yote mpaka ardhi ikawa nyeusi. Wakatafuna
kile chote kilichokuwa kimebakizwa na
ile mvua ya mawe, kila kitu kiotacho
mashambani pamoja na matunda kwenye
miti. Hakuna kitu chochote cha kijani
kilichosalia katika miti au mmea katika
nchi yote ya Misri.
16 [h]Farao akawaita Mose na Aroni kwa
haraka na kuwaambia, “Nimetenda dhambi
dhidi ya BWANA Mungu wenu na dhidi yenu
pia. 17 [i]Sasa unisamehe dhambi yangu mara
moja tena na umwombe BWANA Mungu
wako aondoe pigo hili baya kwangu.”
18 [j]Kisha Mose akaondoka kwa Farao
akamwomba BWANA. 19 Naye BWANA
akaugeuza upepo ukavuma kutoka
magharibi, wenye nguvu nyingi, ambao
uliwaondoa wale nzige na kuwapeleka
kwenye Bahari ya Shamu. Hakuna nzige
hata mmoja aliyebaki popote katika nchi
ya Misri. 20 [k]Lakini BWANA akaufanya moyo
wa Farao kuwa mgumu, wala hakuwaachia
Waisraeli waondoke.

*Pigo La Tisa: Giza*

21 [l]Kisha BWANA akamwambia Mose,
“Nyoosha mkono wako kuelekea angani
ili giza litande katika nchi ya Misri, giza
ambalo watu wanaweza kulipapasa na
kulihisi.” 22 [m]Kwa hiyo Mose akaunyoosha
mkono wake kuelekea angani, na giza nene
likafunika pote katika nchi ya Misri kwa
muda wa siku tatu. 23 [n]Hakuna mtu yeyote
aliyeweza kumwona mwenzake, wala
kuondoka mahali alipokuwa kwa muda wa
siku tatu. Lakini Waisraeli wote walikuwa
na mwanga katika maeneo yao waliyokuwa
wanaishi.

---

[a]**10:7** Kut 23:33; 34:12; Kum 7:16; 12:30; 20:18; Yos 23:13; Amu 2:3; 8:27; 16:5; 1Sam 18:21; Za 106:36; Mhu 7:26; Mwa 20:3; Kut 8:19
[b]**10:8** Kut 8:8
[c]**10:9** Kut 3:18
[d]**10:12** Kut 7:19
[e]**10:13** Kut 4:17; 8:5, 17; 9:23; 14:15-16, 26-27; 17:5; Hes 20:8; 1Fal 8:37; Za 78:46; 105:34; Amo 4:9; Nah 3:16
[f]**10:14** Kum 28:38; Za 78:45; Isa 33:4; Yoe 1:4; 2:1-11, 25; Amo 4:9
[g]**10:15** Kum 28:38; Za 105:34-35; Yoe 1:4; Amo 7:2; Mal 3:11
[h]**10:16** Kut 8:25; 9:27
[i]**10:17** 1Sam 15:25; Kut 8:8
[j]**10:18** Kut 8:30
[k]**10:20** Kut 4:21; 11:10
[l]**10:21** Kum 28:29
[m]**10:22** Za 105:28; Isa 13:10; 45:7; 50:3; Ufu 16:10
[n]**10:23** Kut 8:22; Amo 4:7

[24] [a]Ndipo Farao akamwita Mose na
kusema, “Nendeni, mkamwabudu Bwana.
Hata wanawake na watoto wenu mwaweza
kwenda nao pia, lakini kondoo, mbuzi na
ng’ombe wenu waacheni.”
[25] [b]Lakini Mose akasema, “Huna budi
kuturuhusu tuwe na dhabihu na sadaka
za kuteketezwa za kutoa mbele za Bwana
Mungu wetu. [26] Sisi ni lazima tuondoke
na mifugo yetu pia, wala hakuna ukwato
utakaoachwa nyuma. Inatupasa kutumia
baadhi ya hiyo mifugo katika kumwabudu
Bwana Mungu wetu, kwa kuwa mpaka
tutakapofika huko hatutakuwa tumefahamu
ni nini tutakachotumia katika kumwabudu
Bwana.”
[27] [c]Lakini Bwana akaufanya moyo
wa Farao kuwa mgumu, hakuwa radhi
kuwaachia waondoke. [28] Farao akamwambia
Mose, “Ondoka mbele yangu! Hakikisha
kuwa hutakuja mbele yangu tena! Siku ile
utakapouona uso wangu utakufa.”
[29] [d]Mose akamjibu, “Iwe kama ulivyosema!
Kamwe sitauona uso wako tena.”

### *Pigo La Kumi: Kuuawa Wazaliwa Wa Kwanza*

11 [e]Basi Bwana alikuwa amemwambia
Mose, “Nitaleta pigo moja zaidi kwa
Farao na katika nchi ya Misri. Baada
ya hilo, atawaacha mwondoke hapa na
atakapofanya hivyo, atawafukuza mtoke
kabisa. [2] [f]Waambie watu wote waume
kwa wake wawaombe majirani zao vitu
vya fedha na vya dhahabu.” [3] [g](Bwana
akawafanya Wamisri wawe na moyo
wa ukarimu kwa Waisraeli, naye Mose
mwenyewe akaheshimiwa sana na maafisa
wa Farao na watu wote katika nchi ya
Misri.)
[4] [h]Kwa hiyo Mose akasema, “Hili ndilo
Bwana asemalo: ‘Panapo usiku wa manane
Mimi nitapita katika nchi yote ya Misri.
[5] [i]Kila mwanaume kifungua mimba katika
Misri atakufa, kuanzia mzaliwa wa kwanza
wa kiume wa Farao, aketiye penye kiti cha
ufalme, hadi mzaliwa wa kwanza wa kiume
wa mtumwa wa kike, anayesaga nafaka kwa
jiwe, pamoja na kila mzaliwa wa kwanza wa
mifugo. [6] [j]Patakuwepo kilio kikubwa katika
nchi yote ya Misri, kilio kibaya ambacho
hakijakuwepo wala kamwe hakitakuwepo
tena. [7] [k]Lakini miongoni mwa Waisraeli
hakuna hata mbwa atakayembwekea
mwanadamu wala mnyama yeyote.’ Ndipo
mtakapojua kuwa Bwana huweka tofauti
kati ya Misri na Israeli. [8] [l]Maafisa hawa
wako wote watanijia, wakisujudu mbele
yangu, wakisema, ‘Ondoka, wewe pamoja
na watu wako wote wanaokufuata!’ Baada
ya haya nitaondoka.” Kisha Mose, huku
akiwa amewaka hasira, akamwacha Farao.
[9] [m]Bwana alikuwa amemwambia Mose,
“Farao atakataa kukusikiliza, ili maajabu
yangu yapate kuongezeka katika nchi
ya Misri.” [10] [n]Mose na Aroni wakafanya
maajabu haya yote mbele ya Farao, lakini
Bwana akaufanya moyo wa Farao kuwa
mgumu, wala hakuwaachia Waisraeli
waondoke katika nchi yake.

### *Pasaka*

12 Bwana akamwambia Mose na Aroni
katika nchi ya Misri, [2] [o]“Mwezi huu
utakuwa mwanzo wa miezi kwenu, yaani
mwezi wa kwanza wa mwaka wenu.
[3] [p]Iambie jumuiya yote ya Israeli kwamba
katika siku ya kumi ya mwezi huu, kila
mtu atatwaa mwana-kondoo mmoja kwa
ajili ya familia yake, mmoja kwa kila
nyumba. [4] Ikiwa nyumba yoyote ina watu
wachache wasioweza kumaliza huyo
mwana-kondoo mzima, nyumba hiyo

---

[a]**10:24** Kut 8:8; Mwa 45:10
[b]**10:25** Mwa 8:20; Kut 18:12
[c]**10:27** Kut 4:21; 10:20
[d]**10:29** Kut 11:8; Ebr 11:27
[e]**11:1** Kut 3:20; 6:1
[f]**11:2** Kut 3:21-22
[g]**11:3** Mwa 39:21; Kum 34:11; 2Sam 7:9; 8:13; 22:44; Es 9:4; Za 89:27
[h]**11:4** Kut 12:29; Ay 34:20; Kut 12:23; Za 81:5
[i]**11:5** Kut 4:23; Za 78:51; Isa 47:2
[j]**11:6** Kut 12:30; Mit 21:13; Amo 5:17
[k]**11:7** Kut 8:22
[l]**11:8** Kut 12:31-33; Ebr 11:27
[m]**11:9** Kut 7:4; 3:20
[n]**11:10** Kut 4:21; Rum 2:5
[o]**12:2** Kut 13:4; 23:15; 34:18; 40:2; Kum 16:1; Kut 12:18
[p]**12:3** Mk 14:12; 1Kor 5:7

itabidi ishirikiane na nyumba ya jirani
wa karibu, baada ya kuzingatia idadi ya
watu waliomo. Mtaangalia ni kiasi gani cha
nyama kitahitajika kulingana na mahitaji
ya kila mtu. 5 [a]Wanyama mtakaowachagua,
lazima wawe wa kiume wa umri wa mwaka
mmoja wasiokuwa na dosari, mwaweza
kuwachukua kati ya kondoo au mbuzi.
6 [b]Tunzeni wanyama hao mpaka siku ya
kumi na nne ya mwezi, ambapo lazima
watu wa jumuiya yote ya Israeli wachinje
wanyama hao wakati wa jioni. 7 [c]Ndipo
watakapochukua baadhi ya hiyo damu
na kuipaka kwenye vizingiti vya juu na
miimo ya milango ya nyumba ambamo
watakula wana-kondoo hao. 8 [d]Usiku huo
huo watakula nyama iliyookwa kwenye
moto, pamoja na mboga chungu za majani
na mikate isiyotiwa chachu. 9 [e]Msile nyama
mbichi wala iliyochemshwa, lakini iwe
imeokwa kwenye moto, kichwa, miguu na
nyama zake za ndani. 10 [f]Msibakize nyama
yoyote mpaka asubuhi; nazo kama zitabakia
mpaka asubuhi, lazima mziteketeze kwa
moto. 11 [g]Hivi ndivyo mtakavyokula:
Mtajifunga mikanda viunoni, mtakuwa
mmevaa viatu vyenu miguuni na kushika
fimbo zenu mkononi mwenu. Mle kwa
haraka; hii ni Pasaka ya BWANA.

12 [h]"Usiku huo huo nitapita katika nchi
yote ya Misri na kumuua kila mzaliwa wa
kwanza, wa wanadamu na wa wanyama,
nami nitaihukumu miungu yote ya Misri.
Mimi ndimi BWANA. 13 [i]Damu itakuwa
ishara kwa ajili yenu ya kuonyesha
nyumba ambazo mtakuwamo; nami
nitakapoiona damu, nitapita juu yenu.
Hakuna pigo la uharibifu litakalowagusa
ninyi nitakapoipiga Misri.

14 [j]"Siku hii itakuwa kumbukumbu
kwenu, mtaiadhimisha kuwa sikukuu
kwa BWANA, katika vizazi vyenu vyote:
mtaishika kuwa amri ya kudumu. 15 [k]Kwa
siku saba mtakula mikate isiyotiwa chachu.
Katika siku ya kwanza mtaondoa chachu
yote ndani ya nyumba zenu, kwa maana
yeyote atakayekula chochote chenye chachu
kuanzia siku ya kwanza hadi ya saba lazima
akatiliwe mbali kutoka Israeli. 16 [l]Katika
siku ya kwanza mtakuwa na kusanyiko
takatifu, na kusanyiko jingine katika siku
ya saba. Katika siku hizo msifanye kazi
kamwe isipokuwa kutayarisha chakula cha
kila mmoja; hilo ndilo tu mtakalofanya.

17 [m]"Mtaadhimisha Sikukuu ya Mikate
Isiyotiwa Chachu, kwa sababu hiyo ndiyo
siku ile niliyovitoa vikosi vyenu kutoka
Misri. Mtaiadhimisha siku hii kwa vizazi
vyenu vyote kuwa amri ya kudumu.
18 [n]Katika mwezi wa kwanza mtakula
mikate isiyotiwa chachu, kuanzia jioni ya
siku ya kumi na nne hadi jioni ya siku ya
ishirini na moja. 19 [o]Kwa muda wa siku saba
isionekane chachu yoyote katika nyumba
zenu. Yeyote alaye chochote chenye chachu
ndani yake, lazima akatiliwe mbali kutoka
jumuiya ya Israeli, akiwa ni mgeni au
mzawa. 20 [p]Msile chochote kilichotiwa

---

[a]**12:5** Kut 29:1; Law 1:3; 3:1; 4:3; 22:18-21; 23:12; Hes 6:14; 15:8; 28:3; Kum 15:21; 17:1; Ebr 9:14; 1Pet 1:19
[b]**12:6** Law 23:5; Hes 9:1-11; Yos 5:10; 2Nya 30:2; Kut 16:12; Kum 16:4-6
[c]**12:7** Eze 9:6
[d]**12:8** Kut 16:19; 23:18; 34:25; Law 7:15; Hes 9:11; Kut 13:3; Kum 16:3-7; 2Nya 35:13; 1Kor 5:8
[e]**12:9** Kut 29:13-22; Law 3:3
[f]**12:10** Kut 13:7; 29:34; Law 22:30; Kum 16:4
[g]**12:11** Kum 16:3; Isa 48:20; 52:11; Law 23:5; Hes 9:2-4; 28:16; Kum 16:1; Yos 5:10; 2Fal 23:21-23; 2Nya 30:1; Ezr 6:19; Isa 31:5; Eze 45:21
[h]**12:12** Amo 5:17; Isa 10:33; 31:8; 37:36; Kut 4:23; 13:15; 15:11; 18:11; Hes 33:4; 2Nya 2:5; Za 95:3; 97:9; 135:5; Isa 19:1; Kut 11:4; Yer 43:12; 44:8; Kut 6:2
[i]**12:13** Ebr 11:28; Kut 8:23
[j]**12:14** Kut 13:9; 23:14; 32:5; 13:5, 10; 27:21; Law 3:17; 10:9; 16:29; 23:14; 24; 3; Hes 18:23
[k]**12:15** Kut 13:6-7; 23:15; 34:18; Law 23:6; Hes 28:17; Kum 16:3; 1Kor 5:7; Mwa 17:14; Hes 9:13
[l]**12:16** Hes 29:35
[m]**12:17** Kut 23:15; 34:18; Kum 16:16; 2Nya 8:13; 30:21; Ezr 6:22; Mt 26:17; Lk 22:1; Mdo 12:3; Kut 6:6, 26; 13:3; Law 19:36; 3:17
[n]**12:18** Law 23:5-8; Hes 28:16-25
[o]**12:19** Mwa 17:14; Hes 9:14; 15:14; 35:15; Kum 1:16; Yos 8:33
[p]**12:20** Law 3:17; Hes 35:29; Eze 6:6; Kut 13:6

chachu. Popote muishipo, ni lazima mle
mikate isiyotiwa chachu."
21 [a]Ndipo Mose akawaita wazee wote wa
Israeli na kuwaambia, "Nendeni mara moja
mkachague wanyama kwa ajili ya jamaa
zenu, mkachinje mwana-kondoo wa Pasaka.
22 [b]Chukueni kitawi cha hisopo, kichovyeni
kwenye damu iliyopo kwenye sinia na
kuipaka baadhi ya hiyo damu kwenye
vizingiti na kwenye miimo yote miwili ya
milango. Mtu yeyote asitoke nje ya mlango
wa nyumba yake mpaka asubuhi. 23 [c]Bwana
apitapo katika nchi yote kuwapiga Wamisri,
ataiona damu juu ya vizingiti na kwenye
miimo ya milango, naye atapita juu, wala
hatamruhusu mwangamizi kuingia katika
nyumba zenu na kuwapiga ninyi.
24 "Shikeni maagizo haya yawe kanuni
ya kudumu kwenu na kwa ajili ya wazao
wenu. 25 [d]Mtakapoingia katika nchi
Bwana atakayowapa kama alivyoahidi,
shikeni desturi hii. 26 [e]Watoto wenu
watakapowauliza, 'Sikukuu hii ina maana
gani kwenu?' 27 [f]Basi waambieni, 'Hii ni
dhabihu ya Pasaka kwa Bwana, ambaye
alipita juu ya nyumba za Waisraeli katika
nchi ya Misri na hakudhuru nyumba
zetu alipowapiga Wamisri.' " Ndipo watu
wa Israeli waliposujudu na kuabudu.
28 Waisraeli wakafanya kama vile Bwana
alivyomwagiza Mose na Aroni.
29 [g]Ilipofika usiku wa manane, Bwana
akawapiga wazaliwa wa kwanza wote
katika Misri, kuanzia mzaliwa wa kwanza
wa Farao, mrithi wa kiti cha ufalme,
hadi mzaliwa wa kwanza wa mfungwa,
aliyekuwa gerezani, na wazaliwa wa
kwanza wa mifugo yote pia. 30 [h]Farao,
na maafisa wake wote, na Wamisri wote
wakaamka usiku, na kulikuwa na kilio
kikubwa katika nchi ya Misri, kwa kuwa
haikuwepo nyumba ambayo hakufa mtu.

*Kutoka*

31 [i]Wakati huo Farao akawaita Mose
na Aroni na kuwaambia, "Ondokeni!
Tokeni kwa watu wangu, ninyi pamoja na
Waisraeli! Nendeni mkamwabudu Bwana
kama mlivyoomba. 32 [j]Chukueni makundi
yenu ya kondoo na mbuzi pamoja na
ng'ombe, kama mlivyosema, nanyi mwende
zenu. Nanyi pia mnibariki."
33 [k]Wamisri wakawahimiza Waisraeli
waondoke kwa haraka na kuacha nchi yao.
Kwa kuwa walisema, "La sivyo, tutakufa
wote!" 34 Hivyo watu wakachukua donge
lao la unga kabla ya kutiwa chachu,
wakaweka ndani ya mabakuli ya kukandia,
wakayaviringisha katika vitambaa na
kuyabeba mabegani mwao. 35 [l]Waisraeli
wakafanya kama Mose alivyowaelekeza,
nao wakawaomba Wamisri wawapatie
vitu vya fedha, dhahabu na nguo. 36 [m]Basi
Bwana alikuwa amewafanya Wamisri kuwa
wakarimu kwa hawa watu, wakawapatia
Waisraeli vile walivyotaka kwao; kwa hiyo
wakawateka nyara Wamisri.
37 [n]Waisraeli wakasafiri kutoka Ramesesi
mpaka Sukothi. Walikuwepo wanaume
wapatao 600,000 waendao kwa miguu
bila kuhesabu wanawake na watoto.
38 [o]Watu wengine wengi wakafuatana nao,
pamoja na makundi makubwa ya mifugo
wakiwemo kondoo, mbuzi na ng'ombe.
39 [p]Wakatengeneza maandazi yasiyotiwa
chachu kwa ule unga uliokandwa
waliokuwa wameutoa Misri, donge hilo
la unga halikuwa limetiwa chachu, kwa

[a]**12:21** Mk 14:12-16; Kut 12:11
[b]**12:22** Law 14:4-6; Hes 19:18; Za 51:7; Ebr 11:28; Kut 12:7
[c]**12:23** Isa 19:22; Ufu 7:3; Mwa 16:7; Isa 37:36; Kut 12:7, 13; Yer 6:26; 48:8; 1Kor 10:10; Ebr 11:28
[d]**12:25** Mwa 15:14; Kut 3:17
[e]**12:26** Kut 10:2; 13:8; Yos 4:6
[f]**12:27** Kut 8:23; 12:11; Mwa 24:26; Kut 4:31
[g]**12:29** Kut 11:4; Mwa 19:13; Kut 4:23; 9:6; Za 78:51
[h]**12:30** Kut 11:6
[i]**12:31** Kut 8:8
[j]**12:32** Kut 10:9, 26; Mwa 27:34
[k]**12:33** Kut 6:1; 1Sam 6:6; Mwa 20:3; Kut 8:19; Za 105:38
[l]**12:35** Kut 3:22; Mwa 24:53
[m]**12:36** Mwa 39:21; Kut 3:22
[n]**12:37** Mwa 47:11; Kut 13:20; Hes 33:3-5; Mwa 12:2; Kut 38:26; Hes 1:46; 2:32; 11:13-21; 26:51
[o]**12:38** Hes 11:4; Yos 8:35
[p]**12:39** Kut 3:20; 6:1; 11:1

kuwa walikuwa wameondolewa Misri
kwa haraka nao hawakuwa na muda wa
kuandaa chakula chao.
40 [a]Waisraeli walikuwa wameishi Misri
kwa muda wa miaka 430. 41 [b]Ilikuwa ni siku
ya mwisho ya hiyo miaka 430, vikosi vyote
vya BWANA vilipokuwa vimeondoka Misri.
42 [c]Kwa sababu BWANA aliutenga usiku ule
ili kuwatoa Waisraeli katika nchi ya Misri,
katika usiku huu Waisraeli wote wanapaswa
kuadhimisha kwa kukesha ili kumheshimu
BWANA katika vizazi vijavyo.

*Masharti Kwa Ajili Ya Pasaka*

43 [d]BWANA akamwambia Mose na Aroni,
"Haya ndiyo masharti kwa ajili ya Pasaka:
"Mgeni hataruhusiwa kula Pasaka.
44 [e]Mtumwa yeyote ambaye mmemnunua
aweza kuila kama mmemtahiri, 45 [f]lakini
kibarua yeyote au msafiri haruhusiwi kula.
46 [g]"Sharti iliwe ndani ya nyumba;
msichukue nyama yoyote nje ya nyumba
hiyo. Msiuvunje mfupa wowote. 47 Jumuiya
yote ya Israeli ni lazima waiadhimishe
Pasaka hiyo.
48 [h]"Mgeni aishiye miongoni mwenu
ambaye anataka kuadhimisha Pasaka ya
BWANA ni lazima wanaume wote waliomo
nyumbani mwake wawe wametahiriwa,
ndipo aweze kushiriki kama mzawa.
Mwanaume yeyote asiyetahiriwa
haruhusiwi kuila. 49 [i]Sheria iyo hiyo
itamuhusu mzawa na mgeni anayeishi
miongoni mwenu."
50 Waisraeli wote walifanya kama vile
BWANA alivyomwagiza Mose na Aroni.
51 [j]Siku ile ile BWANA akawatoa Waisraeli
katika nchi ya Misri kwa vikosi vyao.

*Kuwekwa Wakfu Kwa Wazaliwa Wa Kwanza*

13 BWANA akamwambia Mose,
2 [k]"Niwekeeni wakfu kila mzaliwa
wa kwanza wa kiume. Kila mtoto wa
kwanza aliye kifungua tumbo miongoni
mwa Waisraeli ni mali yangu, akiwa wa
mwanadamu au wa mnyama."
3 [l]Ndipo Mose akawaambia watu,
"Ikumbukeni siku hii, siku ambayo
mlitoka katika nchi ya Misri, katika nchi
ya utumwa, kwa sababu BWANA aliwatoa
humo kwa mkono wenye nguvu. Msile
chochote kilichotiwa chachu. 4 [m]Leo, katika
mwezi wa Abibu,[n] mnatoka. 5 [o]BWANA
atakapokuleta katika nchi ya Wakanaani,
Wahiti, Waamori, Wahivi na Wayebusi,
nchi aliyowaapia baba zako kukupa, nchi
itiririkayo maziwa na asali, utaiadhimisha
sikukuu hii katika mwezi huu: 6 [p]Kwa siku
saba utakula mikate isiyotiwa chachu na
katika siku ya saba utamfanyia BWANA
sikukuu. 7 Kwa muda wa siku saba utakula
mikate isiyotiwa chachu, pasionekane
kitu chochote kilicho na chachu miongoni
mwako, wala chachu yoyote isionekane
popote ndani ya mipaka yako. 8 [q]Siku
ile utamwambia mwanao, 'Nafanya hivi
kwa sababu ya jambo ambalo BWANA
alinitendea nilipotoka katika nchi ya Misri.'
9 [r]Adhimisho hili, litakuwa kama alama
kwenye mkono wako na ukumbusho katika
paji lako la uso, kwamba sheria ya BWANA
inapaswa iwe kinywani mwako. Kwa kuwa
BWANA alikutoa katika nchi ya Misri kwa

---

[a]**12:40** Mwa 15:13; Mdo 7:6; Gal 3:17
[b]**12:41** Kut 6:26; 3:10; 12:17
[c]**12:42** Kut 13:10; Law 3:17; Hes 9:3; Kum 16:1, 6
[d]**12:43** Hes 9:14; 15:14; 2Nya 6:32-33; Isa 14:1; 56:3-6; 60:10; Kut 12:11
[e]**12:44** Mwa 17:12-13
[f]**12:45** Law 22:10
[g]**12:46** Hes 9:12; Za 22:14; 34:20; Mit 17:22; Yn 19:36
[h]**12:48** Law 19:18, 34; 24:22; Hes 9:14; 10:32; Eze 44:7
[i]**12:49** Law 24:22; Hes 15:15-16, 29; Kum 1; 16
[j]**12:51** Kut 3:10; 6:6, 26; 12:41
[k]**13:2** Kut 22:29; 34:20; Law 27:26; Hes 3:13; 8:17; 18:15; Kum 15:19; Neh 10:34; Lk 2:23
[l]**13:3** Kut 7:4; Law 26:13; Hes 22:5; 26:4; Kum 4:45; 5:6; Za 81:10; 114:1; Kut 3:20; 12:8
[m]**13:4** Kut 12:2
[n]4 Abibu ni jina la mwezi wa kwanza kwa Wayahudi, ambao ni mwezi wa nne katika kalenda yetu.
[o]**13:5** Kut 3:8; 12:25-26
[p]**13:6** Kut 12:15-20
[q]**13:8** Kut 10:2; Za 78:5-6
[r]**13:9** Isa 44:5; Kum 6:8; 11:18; Mit 3:3; Mt 23:5; Kut 3:20

mkono wake wenye nguvu. 10 [a]Ni lazima
uishike amri hii kwa wakati uliopangwa
mwaka baada ya mwaka.
11 [b]“Baada ya BWANA kukuingiza katika
nchi ya Wakanaani na kukupa nchi
hiyo, kama alivyokuahidi kwa kiapo na
kwa baba zako, 12 [c]inakupasa kumtolea
BWANA mzaliwa wa kwanza wa kila
tumbo. Wazaliwa wote wa kwanza wa
kiume wa mifugo yako ni mali ya BWANA.
13 [d]Kila mzaliwa wa kwanza wa punda
utamkomboa kwa mwana-kondoo, lakini
kama hukumkomboa, utamvunja shingo
yake. Kila mzaliwa wa kwanza mwanaume
miongoni mwa wana wenu utamkomboa.
14 [e]“Katika siku zijazo, mwanao
akikuuliza, ‘Hii ina maana gani?’ Mwambie,
‘Kwa mkono wenye nguvu BWANA alitutoa
katika nchi ya Misri, kutoka nchi ya utumwa.
15 Farao alipokataa kwa ukaidi kuturuhusu
kuondoka, BWANA aliua kila mzaliwa wa
kwanza wa Wamisri, mwanadamu na wa
mnyama. Hii ndiyo sababu ninatoa dhabihu
kwa BWANA mzaliwa wa kwanza wa kiume,
wa kila tumbo na kumkomboa kila mzaliwa
wa kwanza wa wana wangu.’ 16 Jambo hili
litakuwa kama ishara kwenye mkono wako
na kama alama kwenye paji la uso wako,
kwamba BWANA alikutoa katika nchi ya
Misri kwa mkono wake wenye nguvu.”

*Nguzo Ya Wingu Na Moto*

17 [f]Farao alipowaachia watu waende,
Mungu hakuwaongoza kufuata njia
ipitiayo katika nchi ya Wafilisti, ingawa
njia hiyo ilikuwa fupi zaidi. Kwa maana
Mungu alisema, “Wakikabiliana na vita,
wanaweza kubadili mawazo yao na kurudi
Misri.” 18 [g]Kwa hiyo Mungu akawaongoza
watu kupitia njia ya kuzunguka kupitia
jangwani, kuelekea Bahari ya Shamu.
Waisraeli walipanda kutoka nchi ya Misri
wakiwa wamejiandaa kwa vita.
19 [h]Mose akachukua mifupa ya Yosefu kwa
sababu Yosefu alikuwa amewaapisha wana
wa Israeli. Alikuwa amewaambia, “Hakika
Mungu atakuja kuwasaidia, nanyi ni lazima
mwiichukue mifupa yangu mwende nayo
kutoka mahali hapa.”
20 [i]Baada ya Waisraeli kuondoka Sukothi
wakapiga kambi huko Ethamu pembeni
mwa jangwa. 21 [j]Wakati wa mchana
BWANA aliwatangulia kwa nguzo ya wingu
kuwaongoza katika njia yao, na wakati wa
usiku aliwatangulia kwa nguzo ya moto
kuwaangazia, ili waweze kusafiri mchana
au usiku. 22 [k]Ile nguzo ya wingu wakati wa
mchana au ile nguzo ya moto wakati wa
usiku haikuondoka mahali pake mbele ya
watu.

*Kuvuka Bahari Ya Shamu*

14 Ndipo BWANA akamwambia Mose,
2 “Waambie Waisraeli wageuke nyuma
na wapige kambi karibu na Pi-Hahirothi,
kati ya Migdoli na bahari. Watapiga
kambi kando ya bahari, mkabala na
Baal-Sefoni. 3 Farao atafikiri kwamba,
‘Hao Waisraeli wanatangatanga katika
nchi kwa kuchanganyikiwa, nalo jangwa
limewafungia.’ 4 [l]Nami nitaufanya moyo
wa Farao mgumu, naye atawafuatilia.
Lakini nitajipatia utukufu kwa ajili yangu
mwenyewe kupitia Farao na jeshi lake lote,
nao Wamisri watajua kuwa mimi ndimi

[a]**13:10** Kut 12:14; Za 75:2; 102:13
[b]**13:11** Mwa 22:16; Kum 1:8; Mwa 12:7; 17:19; Za 105:42-45
[c]**13:12** Mwa 4:4; Law 27:26; Hes 3:13; 18:15-17; Lk 2:23
[d]**13:13** Law 27:11; Kut 34:20; Isa 66:3; Hes 3:46-47; 18:15
[e]**13:14** Kut 10:2; 20:2; Kum 7:8; 6:20; 28:68
[f]**13:17** Kut 14:11; Hes 14:1-4; Kum 17:16; Hos 11:5
[g]**13:18** Kut 15:22; Za 136:16; Eze 20:10; Yos 4:13
[h]**13:19** Yos 24:32; Mdo 7:16; Ebr 11:22; Mwa 47:29-30
[i]**13:20** Kut 12:37; Hes 33:6
[j]**13:21** Kut 32:1; 33:14; Kum 2:7; 31:8; Amu 4:14; 5:4; Za 68:7; 72:20; Yer 2:2; Hab 3:13; Kut 14:19, 24; 24:16; 33:9-10; 34:5; 40:38; Hes 9:16; 12:5; 14:14; Kum 1:33; Neh 9:12, 19; Za 78:14; 99:7; 105:39; Isa 4:5; 1Kor 10:1
[k]**13:22** Neh 9:19; Hes 33:7; Yer 44:1; Eze 29:10
[l]**14:4** Kut 4:21; Za 71:11; Kut 9:16; Rum 9:17, 22-23; Kut 6:2; 7:5; Eze 32:15

BWANA.” Kwa hiyo Waisraeli wakafanya hivyo.

5 [a]Mfalme wa Misri alipoambiwa kuwa Waisraeli wamekimbia, Farao na maafisa wake wakabadili nia zao kuhusu Waisraeli, wakasema, “Tumefanya nini? Tumewaachia Waisraeli waende zao na tumeukosa utumishi wao!” 6 Kwa hiyo akaandaliwa gari lake la vita, naye akaenda pamoja na jeshi lake. 7 [b]Akachukua magari bora mia sita, pamoja na magari mengine yote ya Misri, pamoja na maafisa wa magari hayo yote. 8 [c]BWANA akaufanya mgumu moyo wa Farao, mfalme wa Misri, kwa hiyo akawafuatia Waisraeli, waliokuwa wakiondoka Misri kwa ujasiri. 9 [d]Nao Wamisri, yaani farasi wote wa Farao na magari ya vita, wapanda farasi na vikosi vya askari, wakawafuatia Waisraeli, wakawakuta karibu na Pi-Hahirothi, mkabala na Baal-Sefoni walipokuwa wamepiga kambi kando ya bahari.

10 [e]Farao alipokaribia, Waisraeli wakainua macho yao, wakawaona Wamisri wakija nyuma yao. Wakashikwa na hofu, wakamlilia BWANA. 11 [f]Wakamwambia Mose, “Je, ni kwamba hayakuwako makaburi huko Misri hata umetuleta tufe huku jangwani? Umetufanyia nini kututoa Misri? 12 [g]Hatukukuambia tulipokuwa huko Misri, tuache tuwatumikie Wamisri? Ingekuwa vyema zaidi kwetu kuwatumikia Wamisri kuliko kufa jangwani!”

13 [h]Mose akawajibu Waisraeli, “Msiogope. Simameni imara, nanyi mtauona wokovu BWANA atakaowapatia leo. Hao Wamisri mnaowaona leo kamwe hamtawaona tena. 14 [i]BWANA atawapigania ninyi, nanyi mnatakiwa kutulia tu.”

15 [j]Ndipo BWANA akamwambia Mose, “Kwa nini wewe unanililia? Waambie Waisraeli waendelee mbele. 16 [k]Inua fimbo yako na unyooshe mkono wako juu ya bahari ili kuyagawa maji, hivyo kwamba Waisraeli wapate kupita mahali pakavu baharini. 17 [l]Nitaifanya mioyo ya Wamisri kuwa migumu kusudi waingie baharini wakiwafuatia. Nami nitajipatia utukufu kupitia Farao pamoja na jeshi lake lote, kupitia magari yake ya vita na wapanda farasi wake. 18 [m]Nao Wamisri watajua kwamba Mimi ndimi BWANA nitakapojipatia utukufu kupitia Farao, magari yake ya vita na wapanda farasi wake.”

19 [n]Ndipo malaika wa Mungu, aliyekuwa akisafiri mbele ya jeshi la Israeli, akaondoka akakaa nyuma yao. Pia ile nguzo ya wingu ikaondoka hapo mbele yao na kusimama nyuma, 20 [o]ikakaa kati ya majeshi ya Misri na Israeli. Usiku kucha wingu likaleta giza upande mmoja na nuru kwa upande mwingine, kwa hiyo hakuna aliyemkaribia mwenzake usiku kucha.

21 [p]Ndipo Mose akanyoosha mkono wake juu ya bahari, naye BWANA akayasukuma maji ya bahari nyuma kwa upepo mkali wa mashariki usiku ule wote na kupafanya

[a]**14:5** Mwa 31:21; Za 105:25
[b]**14:7** Kut 15:4
[c]**14:8** Kut 11:10; Hes 33:2; Mdo 13:17
[d]**14:9** Mwa 47:17; Yos 24:6; Isa 43:17; Kut 15:9
[e]**14:10** Kut 15:25; Yos 24:7; Neh 9:9; Za 5:2; 34:17; 50:15; 107:6, 28
[f]**14:11** Kut 5:21; 16:13; 17:3; Hes 11:1; 14:22; 20:4; 21:5; Kum 9:7
[g]**14:12** Kut 5:21; 15:24; 17:2; Za 106:7-8
[h]**14:13** Mwa 15:1; 1Sam 12:16; 2Nya 20:17; Isa 41:10-14
[i]**14:14** Kut 15:3; Kum 1:30; 3:22; 20:4; Yos 10:14; 23:3; 2Sam 5:24; 2Nya 20:29; Neh 4:20; Za 24:8; Isa 42:13; Yer 41:12; 1Sam 12:16; Za 37:7; 46:10; 116:7; Isa 28:12; 30:15; Zek 2:13
[j]**14:15** Yos 7:10
[k]**14:16** Kut 4:2, 17; Isa 10:26; Hes 20:8-11
[l]**14:17** Kut 4:21
[m]**14:18** Kut 6:2; Eze 32:15
[n]**14:19** Mwa 16:7; Isa 63:9; Kut 13:2; 1Kor 10:1; Isa 26:7; 42:16; 49:10; 52:10; 58:8
[o]**14:20** Yos 24:7
[p]**14:21** Kut 7:19; 4:2; Ay 26:12; Isa 14:27; 23:11; 51:15; Yer 31:35; Mdo 7:36; Mwa 41:6; Kut 15:8; 2Sam 22:16; 1Fal 19:11; Ay 38:1; 40:6; Yer 23:19; Nah 1:3; Mwa 8:1; 2Fal 2:8; Za 74:13; 78:13; 114:5; 136:13; Isa 63:12

nchi kavu. Maji yakagawanyika, [22] [a]nao
Waisraeli wakapita baharini mahali pakavu,
maji yakiwa ukuta upande wao wa kuume
na upande wao wa kushoto.
[23] Wamisri wakawafuatia ndani ya bahari,
pamoja na farasi wote wa Farao, magari
ya vita na wapanda farasi. [24] [b]Karibia
mapambazuko, BWANA akaliangalia jeshi
la Wamisri kutoka ile nguzo ya moto
na ya wingu, akalifadhaisha. [25] [c]Mungu
akayaondoa magurudumu ya magari yao,
kwa hivyo wakayaendesha kwa shida.
Nao Wamisri wakasema, “Tuachane na
Waisraeli! BWANA anawapigania dhidi ya
Misri.”

*Wafuatiaji Wazama*

[26] Ndipo BWANA akamwambia Mose,
“Nyoosha mkono wako juu ya bahari ili
maji yarudiane yawafunike Wamisri,
magari yao ya vita na wapanda farasi
wao.” [27] [d]Mose akanyoosha mkono wake
juu ya bahari, wakati wa mapambazuko
bahari ikarudiana na kuwa kama kawaida.
Wamisri wakajaribu kuyakimbia maji,
lakini BWANA akawasukumia ndani ya
bahari. [28] [e]Maji yakarudiana na kuyafunika
magari ya vita na wapanda farasi pamoja na
jeshi lote la Farao lililokuwa limewafuata
Waisraeli ndani ya bahari. Hakuna hata
mmoja wao aliyenusurika.
[29] [f]Lakini Waisraeli wakapita baharini
mahali pakavu, ukiwepo ukuta wa maji
upande wao wa kuume na upande wao
wa kushoto. [30] [g]Siku ile BWANA akawaokoa
Waisraeli kutoka mikononi mwa Wamisri,
nao Waisraeli wakawaona Wamisri
wamelala ufuoni mwa bahari wakiwa
wamekufa. [31] [h]Basi Waisraeli walipoona
uwezo mkubwa BWANA aliodhihirisha
dhidi ya Wamisri, watu wakamwogopa
BWANA na wakaweka tumaini lao kwake
na kwa Mose mtumishi wake.

*Wimbo Wa Mose Na Miriamu*

15 [i]Ndipo Mose na Waisraeli wakamwimbia
BWANA wimbo huu:

“Nitamwimbia BWANA,
kwa kuwa ametukuzwa sana.
Farasi na mpanda farasi
amewatosa baharini.
[2] [j]BWANA ni nguvu zangu na wimbo
wangu;
amekuwa wokovu wangu.
Yeye ni Mungu wangu, nami
nitamsifu,
Mungu wa baba yangu, nami
nitamtukuza.
[3] [k]BWANA ni shujaa wa vita;
BWANA ndilo jina lake.
[4] [l]Magari ya vita ya Farao na jeshi lake
amewatosa baharini.
Maafisa wa Farao walio bora sana
wamezamishwa katika Bahari ya
Shamu.

---

[a]**14:22** Hes 33:8; Yos 24:6; Isa 43:16; 63:11; 1Kor 10:1; Kut 3:12; 15:19; Kum 31:6-8; Yos 3:16; 4:22; Neh 9:11; Za 66:6; 77:19; 106:9; Isa 11:15; 41:10; 43:5; 44:27; 50:2; 51:10; 63:13; Yer 46:28; Nah 1:4; Ebr 11:29; Kut 15:8; Yos 3:13
[b]**14:24** Kut 13:21; 1Kor 10:1; Kut 23:27; Yos 10:10; 1Sam 5:9; 5:9; 7:10; 14:15; 2Sam 5:24; 2Fal 7:6; 19:7
[c]**14:25** Kum 32:31; 1Sam 2:2; 4:8; Kut 14:14
[d]**14:27** Yos 4:18; Kut 15:1; Kum 1:40; 11:4; Za 78:53; 106:11; 136:15; Ebr 11:29
[e]**14:28** Kut 15:19; Yos 24:7; Kut 15:5; Amu 4:16; Neh 9:11
[f]**14:29** Yos 24:11; 2Fal 2:8; Za 74:15; 78:13
[g]**14:30** 1Sam 14:23; 1Nya 11:14; Za 44:7; 106:8-10; Isa 43:3; 50:2; 51:9-10; 60:16
[h]**14:31** Kut 9:16; Za 147:5; Kut 20:18; Kum 31:13; Yos 4:24; 1Sam 12:18; Za 76:6-7; 112:1; Kut 4:5; Za 22:4; 40:3; 106:12; Yn 2:11; 11:45
[i]**15:1** Hes 21:17; Amu 5:3; 2Sam 22:1; 1Nya 16:9; Ay 36:24; Za 59:16; 105:2; Ufu 15:3; Za 13:6; 21:13; 27:6; 61:8; 104:33; 106:12; Isa 12:5-6; 42:10; 44:23; Kum 11:4; Za 76:6; Yer 51:21; Kut 14:27; Yn 2:11
[j]**15:2** Za 18:1; 59:17; Mwa 45:7; Kut 14:13; Za 18:2, 46; 25:5; 62:2; 118:14; Isa 12:2; 33:2; Yn 2:9; Hab 3:18; Mwa 28:21; Kum 10:21; 2Sam 22:47; Za 22:3; 34:3; 35:27; 99:5; 103:19; 107:32; 108:5; 118:28; 145:11; 148:14; Isa 24:15; Yer 17:14; Dan 4:37
[k]**15:3** Kut 14:14; 3:15; Ufu 19:11
[l]**15:4** Kut 14:6-7; Yer 51:21

5 [a]Maji yenye kina yamewafunika,
wamezama mpaka vilindini kama
jiwe.

6 [b]“Mkono wako wa kuume, Ee
BWANA
ulitukuka kwa uweza.
Mkono wako wa kuume, Ee BWANA,
ukamponda adui.
7 [c]Katika ukuu wa utukufu wako,
ukawaangusha chini wale
waliokupinga.
Uliachia hasira yako kali,
ikawateketeza kama kapi.
8 [d]Kwa pumzi ya pua zako
maji yalijilundika.
Mawimbi ya maji yakasimama imara
kama ukuta,
vilindi vikagandamana ndani ya
moyo wa bahari.

9 [e]“Adui alijivuna,
‘Nitawafuatia, nitawapata.
Nitagawanya nyara;
nitajishibisha kwa wao.
Nitafuta upanga wangu
na mkono wangu utawaangamiza.’
10 [f]Lakini ulipuliza kwa pumzi yako,
bahari ikawafunika.
Wakazama kama risasi
kwenye maji makuu.

11 [g]“Ni nani miongoni mwa miungu
aliye kama wewe, Ee BWANA?
Ni nani kama Wewe:
uliyetukuka katika utakatifu,
utishaye katika utukufu,
ukitenda maajabu?
12 [h]Uliunyoosha mkono wako wa
kuume
na nchi ikawameza.

13 [j]“Katika upendo wako usiokoma
utawaongoza
watu uliowakomboa.
Katika nguvu zako utawaongoza
mpaka makao yako matakatifu.
14 [k]Mataifa watasikia na kutetemeka,
uchungu utawakamata watu wa
Ufilisti.
15 [l]Wakuu wa Edomu wataogopa,
viongozi wa Moabu watatetemeka
kwa hofu,
watu wa Kanaani watayeyuka,
16 [m]vitisho na hofu vitawaangukia.
Kwa nguvu ya mkono wako
watatulia kama jiwe,
mpaka watu wako waishe kupita, Ee
BWANA,
mpaka watu uliowanunua wapite.
17 [n]Utawaingiza na kuwapandikiza
juu ya mlima wa urithi wako:
hapo mahali, Ee BWANA,

---

[a]**15:5** Kut 14:28; Neh 9:11
[b]**15:6** Za 16:11; 17:7; 21:8; 63:8; 74:11; 77:10; 89:13; 118:15; 138:7; Kut 3:20; Ay 40:14; Hes 24:8; 1Sam 2:10; Za 2:9
[c]**15:7** Kum 33:26; Za 150:2; 2:5; 78:49-50; Yer 12:13; 25:38; Kut 24:17; Kum 4:24; 9:3; Za 18:8; 59:13; Ebr 12:29
[d]**15:8** Kut 14:21; Za 18:15; Yos 3:13; Za 78:13; Isa 43:16; Kut 14:22; Za 46:2
[e]**15:9** Kut 14:5-9; Kum 28:45; Za 7:5; Mao 1:3; Amu 5:30; Isa 9:3; 53:12; Lk 11:22
[f]**15:10** Neh 9:11; Za 32:6; Ay 4:9; 15:30; Isa 11:4; 30:33; 40:7; Za 29:3
[g]**15:11** Kut 8:10; Za 77:13; 99:3; 110:3; 4:2; 26:8; Isa 46:5; 35:2; 40:5; Law 19:2; 1Sam 2:2; 1Nya 16:29; Isa 6:3; Ufu 4:8; Kut 3:20
[h]**15:12** Kut 7:5; Hes 16:32; 26:10; Kum 11:6; Za 106:17
[j]**15:13** Neh 9:12; Za 77:20; Kut 6:6; Ay 33:28; Za 71:23; 106:10; Isa 1:27; 41:14; 43:14; 44:22-24; 51:10; 63:9; Tit 2:14; Za 68:16; 76:2; 78:54
[k]**15:14** Kut 23:27; Kum 2:25; Yos 2:9; 9:24; 1Sam 4:7; Es 8:17; Za 48:6; 96:9; 99:1; 114:7; Eze 38:20; Isa 13:8; Za 83:7
[l]**15:15** Mwa 36:15; Kum 2:4; Hes 22:3; Za 114:7; Yos 2:9, 24
[m]**15:16** Mwa 35:5; 1Sam 25:37; Za 74:2; 2Pet 2:1-2; Kum 2:4; Yos 2:9
[n]**15:17** Kut 23:20; 32:34; 33:12; 2Sam 7:10; Za 44:2; 80:8; Isa 5:2; 60:21; Yer 2:21; 11:17; 24:6; Amo 9:15; Kum 33:19; Za 2:6; 3:4; 78:54-68; 133:3; Dan 9:16; Yoe 2:1; Oba 1:16; Sef 3:11; Za 132:13-14; 78:69; 114:2

ulipopafanya kuwa makao
yako,
mahali patakatifu, Ee BWANA,
ulipopajenga kwa mikono
yako.
18 [a]BWANA atatawala
milele na milele."

19 [b]Farasi wa Farao, magari yake ya
vita na wapanda farasi wake walipoingia
baharini, BWANA aliyarudisha maji ya
bahari yakawafunika, lakini wana wa Israeli
walipita baharini mahali pakavu. 20 [c]Kisha
Miriamu yule nabii mke, ndugu yake
Aroni, akachukua matari mkononi mwake
na wanawake wote wakamfuata na matari
yao wakicheza. 21 [d]Miriamu akawaimbia:

"Mwimbieni BWANA,
kwa maana ametukuka sana.
Farasi na mpanda farasi
amewatosa baharini."

*Maji Ya Mara Na Elimu*

22 [e]Kisha Mose akawaongoza Israeli
kutoka Bahari ya Shamu na kuingia katika
Jangwa la Shuri. Kwa siku tatu walisafiri
jangwani bila kupata maji. 23 [f]Walipofika
Mara, hawakuweza kunywa maji yake kwa
sababu yalikuwa machungu. (Ndiyo sababu
mahali hapo panaitwa Mara[g]) 24 [h]Kwa hiyo
watu wakamnung'unikia Mose, wakisema,
"Tunywe nini?"
25 [i]Ndipo Mose akamlilia BWANA, naye
BWANA akamwonyesha kipande cha mti.
Akakitupa ndani ya maji, nayo maji yakawa
matamu.

Huko BWANA akawapa amri na sheria
na huko akawajaribu. 26 [j]Mungu akasema,
"Kama mkisikiliza kwa bidii sauti ya
BWANA Mungu wenu na kuyafanya yaliyo
sawa machoni pake, kama mkiyatii maagizo
yake na kuzishika amri zake zote, sitaleta
juu yenu ugonjwa wowote niliowaletea
Wamisri, kwa kuwa Mimi ndimi BWANA,
niwaponyaye."
27 [k]Kisha wakafika Elimu, mahali
palipokuwa na chemchemi kumi na mbili,
na miti sabini ya mitende, wakapiga kambi
huko karibu na maji.

*Mana Na Kware*

16 [l]Jumuiya yote ya Kiisraeli ikaondoka
Elimu, wakafika Jangwa la Sini,
lililokuwa kati ya Elimu na Sinai, siku
ya kumi na tano ya mwezi wa pili baada
ya kutoka Misri. 2 [m]Huko jangwani hiyo
jumuiya yote wakawanung'unikia Mose
na Aroni. 3 [n]Waisraeli wakawaambia, "Laiti
tungelikufa kwa mkono wa BWANA huko
Misri! Huko tuliketi tukizunguka masufuria
ya nyama na tukala vyakula tulivyovitaka,
lakini ninyi mmetuleta huku jangwani ili
mpate kuua mkutano huu wote kwa njaa."
4 [o]Kisha BWANA akamwambia Mose,
"Nitanyesha mikate kutoka mbinguni
kwa ajili yenu. Watu watatoka kila siku
na kukusanya kitakachowatosha kwa siku
ile, kwa njia hii, nitawajaribu nione kama

[a]**15:18** Mwa 21:33; Za 9:7; 29:10; 55:19; 66:7; 80:1; 102:12; 145:13; Mao 5:19
[b]**15:19** Kut 14:28; 14:22
[c]**15:20** Kut 2:4; Hes 12:1; 20:1; 26:59; 1Nya 4:17; 6:3; Amu 4:4; 2Fal 22:14; 2Nya 34:22; Neh 6:14; Isa 8:3; Eze 13:17; Mwa 31:27; 1Sam 18:6; Za 81:2; Isa 30:32; Mwa 4:21; Amu 11:34; 21:21; 2Sam 6:8-16; Za 30:11; 149:3; Wim 6:13; Yer 31:4, 13
[d]**15:21** 1Sam 18:17; Amo 2:15; Hag 2:22; Kut 14:27; 15:1
[e]**15:22** Za 78:52; Mwa 16:7; Kut 17:1-3; Hes 20:2-5; 33:14; Za 107:5
[f]**15:23** Hes 33:8; Rut 1:20
[g]23 Mara maana yake ni Chungu.
[h]**15:24** Kut 14:12; 16:2; Hes 14:2; Yos 9:18; Za 78:18, 42; 106:13, 25; Eze 16:43; Mt 6:31
[i]**15:25** Kut 14:10; 2Fal 2:21; 4:41; Amu 3:4; Ay 23:10; Za 81:7; Isa 48:10
[j]**15:26** Kut 32:22; Kum 11:13; 15:5; Yer 11:6; Kut 19:5-6; 20:2-7; Kum 7:12, 15; 28:27, 58; 32:39; 1Sam 5:6; Za 30:2; 41:3-4; 103:3; Kut 23:25-26; 2Fal 20:5; Za 25:11; 107:20; Yer 30:17; Hos 11:3
[k]**15:27** Hes 33:9
[l]**16:1** Kut 17:1; Hes 33:11-12; Kut 6:6; 12:1-2
[m]**16:2** Kut 15:24; 14:11; 1Kor 10:10
[n]**16:3** Kut 17:3; Hes 14:2; 20:3; 11:4, 34; Kum 12:20; Za 78:18; 106:14; Yer 44:12; Mwa 47:15
[o]**16:4** Dan 8:3; Neh 9:15; Za 78:24; 105:40; Yn 6:31; Mwa 22:1

watafuata maelekezo yangu. 5 [a]Siku ya
sita watatayarisha kile waletacho ndani,
nacho kitakuwa mara mbili kuliko ya kile
walichokusanya kila siku.”
6 [b]Kwa hiyo Mose na Aroni wakawaambia
Waisraeli wote, “Jioni mtajua kwamba
BWANA ndiye aliwatoa Misri, 7 [c]kisha
asubuhi mtauona utukufu wa BWANA, kwa
sababu amesikia manung’uniko yenu dhidi
yake. Sisi ni nani hata mtunung’unikie?”
8 [d]Pia Mose akasema, “Mtajua kuwa
alikuwa BWANA wakati atakapowapa
nyama mle ifikapo jioni na mikate yote
mtakayohitaji asubuhi kwa sababu amesikia
manung’uniko yenu dhidi yake. Sisi ni
nani? Hamnung’uniki dhidi yetu, bali dhidi
ya BWANA.”
9 Kisha Mose akamwambia Aroni, “Iambie
jumuiya yote ya Waisraeli kwamba, ‘Mje
mbele zake BWANA, kwa maana amesikia
manung’uniko yenu.’ ”
10 [e]Aroni alipokuwa akizungumza na
jumuiya yote ya Waisraeli, wakatazama
kuelekea jangwani, na huko wakaona
utukufu wa BWANA ukitokeza katika wingu.
11 BWANA akamwambia Mose,
12 [f]“Nimesikia manung’uniko ya Waisraeli.
Waambie, ‘Jioni mtakula nyama, na asubuhi
mtashiba mikate. Ndipo mtajua ya kwamba
Mimi ndimi BWANA Mungu wenu.’ ”
13 [g]Jioni ile kware wakaja wakaifunika
kambi na asubuhi kulikuwa na tabaka
la umande kuzunguka kambi. 14 [h]Wakati
umande ulipoondoka, vipande vidogo
vidogo kama theluji vilionekana juu ya
uso wa jangwa. 15 [i]Waisraeli walipoona,
wakaambiana, “Hiki ni nini?” Kwa kuwa
hawakujua kilikuwa kitu gani.
Mose akawaambia, “Huu ndio mkate
ambao BWANA amewapa mle. 16 Hivi
ndivyo BWANA alivyoamuru: ‘Kila mmoja
akusanye kiasi anachohitaji. Chukueni
pishi[j] moja kwa kila mtu mliye naye katika
hema yenu.’ ”
17 Waisraeli wakafanya kama
walivyoambiwa, baadhi yao wakakusanya
zaidi, wengine pungufu. 18 [k]Nao walipopima
katika pishi, yule aliyekusanya zaidi
hakuwa na ziada, wala aliyekusanya kidogo
hakupungukiwa. Kila mmoja alikusanya
kiasi alichohitaji.
19 [l]Kisha Mose akawaambia, “Mtu yeyote
asibakize chochote mpaka asubuhi.”
20 [m]Hata hivyo, wengine hawakuzingatia
aliyosema Mose, wakahifadhi kiasi fulani
mpaka asubuhi, lakini kile alichohifadhi
kikajaa mabuu na kuanza kunuka. Kwa hiyo
Mose akawakasirikia.
21 Kila asubuhi, kila mmoja alikusanya
kiasi alichohitaji na jua lilipokuwa kali,
iliyeyuka. 22 [n]Siku ya sita, wakakusanya
mara mbili, kiasi cha pishi mbili kwa kila
mtu, nao viongozi wa jumuiya wakaja
kumwarifu Mose. 23 [o]Mose akawaambia,
“Hivi ndivyo alivyoagiza BWANA: ‘Kesho
itakuwa siku ya mapumziko, Sabato
takatifu kwa BWANA. Kwa hiyo okeni
kile mnachotaka kuoka na mchemshe
kile mnachotaka kuchemsha. Hifadhini
chochote kinachobaki na mkiweke mpaka
asubuhi.’ ”
24 Kwa hiyo wakavihifadhi mpaka
asubuhi, kama Mose alivyoagiza, na
havikunuka wala kuwa na mabuu. 25 Mose
akawaambia, “Kuleni leo, kwa sababu
leo ni Sabato kwa BWANA. Hamtapata

[a]**16:5** Law 25:21
[b]**16:6** Kut 6:6
[c]**16:7** Kut 24:16; 29:43; 33:18-22; 40:34; Law 9:6; Hes 16:19; Kum 5:24; 1Fal 8:11; Za 63:2; Isa 6:3; 35:2; 40:5; 44:23; 66:18; Eze 1:28; 10:4; 43:5; Hab 2:14; Hag 2:7; Yn 11:40; Hes 11:1; 17:5; 16:11
[d]**16:8** Hes 23:21; Kum 33:5; Amu 8:23; 1Sam 8:17; 12:12; Mt 10:40; Rum 13:2; 1The 4:8
[e]**16:10** Yn 11:2; Kut 13:21; 40:34-35; 1Fal 8:10; 2Nya 7:1; Eze 10:4
[f]**16:12** Kut 6:2; 16:7; 20:2
[g]**16:13** Hes 11:31; Za 78:27-28; 105:40; 106:15; Hes 11:9
[h]**16:14** Hes 11:7-9; Kum 8:3, 16; Za 105:40
[i]**16:15** Kum 8:16; Neh 9:20; Yn 6:31
[j]16 Pishi ni kipimo cha ujazo, kwa Kiebrania ni omeri, ambacho ni sawa na kilo mbili.
[k]**16:18** 2Kor 8:15
[l]**16:19** Kut 12:10; 23:18
[m]**16:20** Kut 32:31
[n]**16:22** Kut 34:31
[o]**16:23** Mwa 2:3; Kut 20:8; Kum 5:13-14

chochote juu ya nchi leo. 26 [a]Kwa siku sita mtakusanya, lakini siku ya saba, yaani Sabato, hakutakuwepo chochote.”

27 Hata hivyo, baadhi ya watu wakatoka kwenda kukusanya siku ya saba, lakini hawakupata chochote. 28 [b]Ndipo BWANA akamwambia Mose, “Je, mtaacha kushika maagizo na maelekezo yangu mpaka lini? 29 Fahamuni kuwa BWANA amewapa ninyi Sabato, ndiyo sababu katika siku ya sita amewapa mikate ya siku mbili. Kila mmoja inampasa kukaa pale alipo katika siku ya saba. Hata mmoja haruhusiwi kutoka.” 30 Kwa hiyo watu wakapumzika siku ya saba.

31 Watu wa Israeli wakaita ile mikate mana[c] Ilikuwa myeupe kama mbegu za mtama na ladha yake ilikuwa kama mkate mwembamba uliotengenezwa kwa asali. 32 Mose akasema, “Hivi ndivyo alivyoagiza BWANA: ‘Chukueni pishi ya mana na kuhifadhi kwa ajili ya vizazi vijavyo ili vione mikate niliyowapa mle jangwani nilipowatoa katika nchi ya Misri.’ ”

33 [d]Kwa hiyo Mose akamwambia Aroni, “Chukua gudulia na uweke pishi moja ya mana ndani yake. Kisha uweke mbele za BWANA ili kihifadhiwe kwa ajili ya vizazi vijavyo.”

34 [e]Kama BWANA alivyomwagiza Mose, hatimaye Aroni alikuja kuihifadhi ndani ya Sanduku la Ushuhuda. 35 [f]Waisraeli wakala mana kwa miaka arobaini, mpaka walipofika katika nchi iliyokaliwa na watu; walikula mana hadi walipofika mpakani mwa Kanaani.

36 [g](Pishi moja ni sehemu ya kumi ya kipimo cha efa.[h])

*Maji Kutoka Kwenye Mwamba*

**(Hesabu 20:1-13)**

17 [i]Jumuiya yote ya Israeli ikaondoka kutoka Jangwa la Sini, ikisafiri kutoka sehemu moja hadi nyingine kama BWANA alivyoagiza. Wakapiga kambi huko Refidimu, lakini hapakuwa na maji ya watu kunywa. 2 [j]Kwa hiyo wakagombana na Mose wakisema, “Tupe maji ya kunywa.”

Mose akajibu, “Mbona mnagombana nami? Kwa nini mnamjaribu BWANA?”

3 [k]Lakini watu walikuwa na kiu huko, wakanung’unika dhidi ya Mose, wakisema, “Kwa nini ulitutoa kule Misri, ukatuleta hapa utuue kwa kiu sisi, watoto wetu na mifugo yetu?”

4 [l]Kisha Mose akamlilia BWANA, akasema, “Niwafanyie nini watu hawa? Sasa wanakaribia kunipiga kwa mawe.”

5 [m]BWANA akamjibu Mose, “Pita mbele ya watu. Wachukue pamoja nawe baadhi ya wazee wa Israeli, ichukue mkononi mwako ile fimbo uliyopiga nayo Mto Naili, nawe uende. 6 [n]Huko nitasimama mbele yako karibu na mwamba wa Horebu. Uupige mwamba na maji yatatoka ndani yake kwa ajili ya watu kunywa.” Kwa hiyo Mose akafanya haya mbele ya wazee wa Israeli. 7 [o]Naye akapaita mahali pale Masa,[p] na Meriba[q] kwa sababu Waisraeli waligombana

---

[a]**16:26** Kut 20:9-10
[b]**16:28** Yos 9:14; Za 78:10; 106:13; 107:11; Yer 32:23; 2Fal 17:14
[c]31 Mana maana yake ni mkate kutoka mbinguni.
[d]**16:33** Ebr 9:4; Ufu 2:17
[e]**16:34** Kut 25:16, 21-22; 27:21; 31:18; 40:20; Law 16:13; Hes 1:50; 7:89; 10:11; 17:4; Kum 2:10; 1Fal 8:9; 2Nya 5:10
[f]**16:35** Yn 6:31, 49; Hes 14:33; 33:38; Kum 1:3; 2:7; 8:2-4; Yos 5:6; Amu 3:11; Neh 9:21; Za 95:10; Amu 5:25; Yos 5:12
[g]**16:36** Law 5:11; 6:20; Hes 5:15; 15:4; 28:5
[h]36 Efa moja ni sawa na kilo 22.
[i]**17:1** Kut 16:1; 19:2; Hes 3:15; 20:5; 33:14
[j]**17:2** Hes 20:2; 33:14; Za 107:5; Kut 14:12; Kum 6:16; Za 78:18, 41; 106:14; Mt 4:7; 1Kor 10:9
[k]**17:3** Kut 15:22-24; 14:11; 16:2-3
[l]**17:4** Hes 14:10; Isa 30:6; Yn 8:59
[m]**17:5** Kut 4:2; 10:12-13; 7:20
[n]**17:6** Hes 20:8-11; Kum 8:15; Amu 15:19; 2Fal 3:20; Neh 9:15; Za 74:15; 78:15-16; 105:41; 107:35; 114:8; Isa 30:25; 35:6; 43:19; 48:21; 1Kor 10:4
[o]**17:7** Kum 6:16; 9:22; 33:8; Za 95:8; Hes 20:13, 24; 27:14; Za 81:7; 106:32
[p]7 Masa maana yake ni Kujaribu.
[q]7 Meriba maana yake ni Kugombana.

na kumjaribu BWANA wakisema, “Je,
BWANA yu pamoja nasi au la?”

*Vita Na Waamaleki*

8 [a]Waamaleki wakaja na kuwashambulia
Waisraeli huko Refidimu. 9 [b]Mose
akamwambia Yoshua, “Chagua baadhi
ya watu wetu na uende kupigana na
Waamaleki. Kesho nitasimama juu ya
kilima nikiwa na fimbo ya Mungu mkononi
mwangu.”
10 [c]Kwa hiyo Yoshua akapigana na
Waamaleki kama Mose alivyomwagiza,
nao Mose, Aroni na Huri wakapanda juu
ya kilima. 11 [d]Ikawa wakati wote Mose
alipokuwa amenyanyua mikono yake,
Waisraeli walikuwa wakishinda, lakini
kila aliposhusha mikono yake Waamaleki
walishinda. 12 [e]Mikono ya Mose ilipochoka,
wakachukua jiwe na kumpa alikalie. Aroni
na Huri wakaishikilia juu mikono ya Mose,
mmoja upande huu na mwingine upande
huu. Wakaitegemeza mikono yake ikabaki
thabiti mpaka jua lilipozama. 13 Kwa hiyo
Yoshua akalishinda jeshi la Waamaleki kwa
upanga.
14 [f]Kisha BWANA akamwambia Mose,
“Andika mambo haya katika kitabu ili
yakumbukwe, na uhakikishe kwamba
Yoshua amesikia, kwa sababu nitafuta
kabisa kumbukumbu la Amaleki chini ya
mbingu.”
15 [g]Mose akajenga madhabahu na kuiita
Yehova Nisi.[h] 16 [i]Mose akasema, “Kwa
maana mikono iliinuliwa mpaka kwenye
kiti cha enzi cha BWANA. BWANA atakuwa
na vita dhidi ya Waamaleki kutoka kizazi
hata kizazi.”

*Yethro Amtembelea Mose*

18 [j]Basi Yethro, kuhani wa Midiani,
baba mkwe wa Mose, akawa amesikia
kila kitu Mungu alichomfanyia Mose na
watu wake wa Israeli, pia jinsi BWANA
alivyowatoa Israeli Misri.
2 [k]Baada ya Mose kumrudisha mkewe
Sipora, Yethro baba mkwe wake alimpokea
3 [l]pamoja na wanawe wawili. Jina la mmoja
aliitwa Gershomu, kwa kuwa Mose alisema,
“Nimekuwa mgeni katika nchi ya kigeni.”
4 [m]Mwingine aliitwa Eliezeri, kwa kuwa
alisema, “Mungu wa baba yangu alikuwa
msaada wangu, akaniokoa kutoka upanga
wa Farao.”
5 [n]Yethro, baba mkwe wa Mose, pamoja na
wana wawili wa Mose na mkewe, wakamjia
Mose huko jangwani, mahali alipokuwa
amepiga kambi karibu na mlima wa Mungu.
6 Yethro alikuwa ametuma ujumbe kwake
Mose, kusema, “Mimi Yethro baba mkwe
wako ninakuja kwako pamoja na mke wako
na wanao wawili.”
7 [o]Kwa hiyo Mose akatoka kumlaki
baba mkwe wake, akainama na kumbusu.
Wakasalimiana, kisha wakaingia hemani.
8 [p]Mose akamwambia baba mkwe wake
kuhusu kila kitu BWANA alichomfanyia
Farao na Wamisri kwa ajili ya Israeli, na
pia kuhusu shida zote walizokutana nazo
njiani na jinsi BWANA alivyowaokoa.
9 [q]Yethro akafurahishwa sana kusikia
juu ya mambo yote mazuri BWANA
aliyowatendea Waisraeli kuwaokoa kutoka
mkono wa Wamisri. 10 [r]Yethro akasema,
“Sifa na ziwe kwa BWANA, aliyekuokoa

[a]**17:8** Mwa 36:12; Kum 25:17-19
[b]**17:9** Kut 24:13; 32:17; 33:11; Hes 11:28; 27:22; Kum 1:38; Mdo 7:45; Kut 4:17
[c]**17:10** Kut 24:14; 31:2
[d]**17:11** Yak 5:16
[e]**17:12** Yos 8:26
[f]**17:14** Kut 24:4; 34:27; 33:2; Kum 31:9; Ay 19:23; Isa 30:8; Yer 36:2; 45:1; 51:60; Kut 32:33; Kum 29:20; Ay 18:17; Za 9:5; 34:15; 109:15; Eze 18:4; Mwa 36:12; Hes 24:7; Amu 3:13; Isa 30:17-18; Za 83:7
[g]**17:15** Mwa 8:20; 22:14
[h]15 Yehova Nisi maana yake ni BWANA ni Bendera yangu.
[i]**17:16** Hes 24:7; 1Sam 15:8, 32; 1Nya 4:43; Es 3:1; 8:3; 9:5, 24
[j]**18:1** Kut 12:16-18; 6:6
[k]**18:2** Kut 2:21
[l]**18:3** Kut 4:20; Mdo 7:29; Kut 2:22
[m]**18:4** 1Nya 23:15; Mwa 49:25; Kum 33:29
[n]**18:5** Kut 3:1
[o]**18:7** Mwa 17:3; 43:8; 29:13
[p]**18:8** Hes 20:14; Neh 9:32; Kut 15:5, 16; Za 81:7
[q]**18:9** Yos 21:45; 1Fal 8:66; Neh 9:25; Isa 63:7
[r]**18:10** Mwa 9:26; 24:27

wewe kutoka mikononi mwa Wamisri
na Farao, na aliyewaokoa watu kutoka
mikononi mwa Wamisri. 11 [a]Sasa najua
ya kuwa BWANA ni mkuu kuliko miungu
mingine yote, kwa kuwa amewatendea hivi
wale waliowatenda Israeli kwa ujeuri."
12 [b]Kisha Yethro, baba mkwe wa Mose,
akaleta sadaka ya kuteketezwa na dhabihu
nyingine kwa Mungu, naye Aroni pamoja na
wazee wote wa Israeli wakaja kula chakula
pamoja na baba mkwe wa Mose mbele za
Mungu.

*Ushauri Wa Yethro*

**(Kumbukumbu 1:9-18)**

13 Siku iliyofuata, Mose akachukua
nafasi yake kama hakimu wa watu, nao
wakasimama kumzunguka kuanzia asubuhi
hadi jioni. 14 Baba mkwe wake alipoona yote
Mose anayowafanyia watu, akasema, "Ni
nini hiki unachowafanyia watu? Kwa nini
wewe unakuwa mwamuzi wa watu hawa
peke yako, wakati watu hawa wamesimama
wakikuzunguka tangu asubuhi mpaka
jioni?"
15 [c]Mose akamjibu, "Kwa sababu watu
wananijia kutaka mapenzi ya Mungu.
16 [d]Kila wakiwa na shauri huletwa kwangu,
nami huamua kati ya mtu na mwenzake
na kuwajulisha juu ya amri na sheria za
Mungu."
17 Baba mkwe wa Mose akamjibu,
"Unachofanya sio kizuri. 18 [e]Wewe pamoja
na watu hawa wanaokujia mtajichosha
bure. Kazi ni nzito sana kwako, huwezi
kuibeba mwenyewe. 19 [f]Sasa nisikilize
mimi, nitakupa shauri, naye Mungu na awe
pamoja nawe. Yapasa wewe uwe mwakilishi
wa watu mbele za Mungu na ulete mashauri
yao kwake. 20 [g]Uwafundishe amri na sheria,
tena uwaonyeshe namna ya kuishi na kazi
zinazowapasa wao kufanya. 21 [h]Lakini
uchague watu wenye uwezo miongoni
mwa watu wote, watu wanaomwogopa
Mungu, watu waaminifu wanaochukia mali
ya dhuluma, uwateuwe wawe maafisa juu
ya maelfu, mamia, hamsini na makumi.
22 [i]Waweke wawe waamuzi wa watu kwa
wakati wote, lakini waambie wakuletee
kila shauri lililo gumu; yale yaliyo rahisi
wayaamue wao wenyewe. Hii itafanya
mzigo wako kuwa mwepesi, kwa sababu
watashirikiana nawe. 23 Kama ukifanya hivi,
na ikiwa Mungu ameagiza hivyo, utaweza
kushinda uchovu, nao watu hawa wote
watarudi nyumbani wameridhika."

*Kuchaguliwa Kwa Waamuzi*

24 Mose akamsikiliza baba mkwe wake
na kufanya kila kitu alichosema. 25 [j]Mose
akawachagua watu wenye uwezo kutoka
Israeli yote, akawafanya kuwa viongozi
wa watu, maafisa juu ya maelfu, mamia,
hamsini na makumi. 26 [k]Wakatumika kama
waamuzi wa watu kwa wakati wote.
Mashauri magumu wakayaleta kwa Mose,
lakini yale yaliyo rahisi wakayaamua
wenyewe.
27 [l]Kisha Mose akaagana na Yethro baba
mkwe wake, naye akarudi kwa nchi yake.

*Waisraeli Kwenye Mlima Sinai*

19 [m]Mnamo mwezi wa tatu baada ya
Waisraeli kuondoka Misri, siku kama
iyo hiyo, wakafika katika Jangwa la Sinai.

---

[a]**18:11** Kut 12:12; 1Nya 16:25; Kut 1:10; Lk 1:51
[b]**18:12** Kut 3:1; 10:25; 20:24; Law 1:2-9; Mwa 31:54; Kut 24:5; Mwa 26:30; Kum 12:7
[c]**18:15** Mwa 25:22; Hes 9:6-8
[d]**18:16** Kut 24:14; Law 24:12; Hes 15:34; Kum 1:17; 2Nya 19:7; Mit 24:23; Mt 2:9
[e]**18:18** Hes 11:11, 14, 17; Kum 1:9-12
[f]**18:19** Kut 3:12; Hes 27:5
[g]**18:20** Kum 4:1-4; 5:1; Za 119:12, 26, 68; 143:8; Mwa 39:11
[h]**18:21** Mwa 47:6; Mdo 6:3; Mwa 22:12; Kut 23:8; Kum 16:19; 1Sam 12:3; Za 15:5; Mit 17:23; 28:8; Mhu 7:7; Eze 18:8; 22:12; Hes 1:16; 7:2; 10:4; Kum 16:18; Ezr 7:25
[i]**18:22** Law 24:11; Kum 17:18; Hes 11:17; Kum 1:9
[j]**18:25** Hes 1:16; 7:2; 11:16; Kum 16:18; 1:13-15
[k]**18:26** Kum 16:18; 2Nya 19:5; Ezr 7:25; Kum 1:17
[l]**18:27** Hes 10:29-30
[m]**19:1** Kut 6:6; Hes 3:14; 33:15

2 [a]Baada ya kuondoka Refidimu, waliingia
katika Jangwa la Sinai na Israeli wakapiga
kambi pale jangwani mbele ya mlima.
3 [b]Kisha Mose akakwea kwenda kwa
Mungu, naye BWANA akamwita kutoka
kwenye ule mlima akasema, “Hivi ndivyo
utakavyosema na nyumba ya Yakobo na
utakachowaambia watu wa Israeli: 4 [c]‘Ninyi
wenyewe mmeona nililofanya huko Misri,
jinsi nilivyowabeba kwenye mbawa za tai
na kuwaleta kwangu. 5 [d]Sasa kama mkinitii
kikamilifu na kutunza Agano langu, basi
ninyi mtakuwa mali yangu ya thamani
kubwa miongoni mwa mataifa yote.
Ijapokuwa dunia yote ni mali yangu, 6 [e]ninyi
mtakuwa kwangu ufalme wa makuhani
na taifa takatifu.’ Haya ndiyo maneno
utakayosema kwa wana wa Israeli.”
7 [f]Kwa hiyo Mose akarudi, akawaita
wazee wa watu na kuwaambia maneno yote
ambayo BWANA alikuwa amemwamuru
ayaseme. 8 [g]Watu wote wakajibu kwa
pamoja, “Tutafanya kila kitu BWANA
alichokisema.” Naye Mose akarudisha
majibu yao kwa BWANA.
9 [h]BWANA akamwambia Mose,
“Nitakujia katika wingu zito, ili watu
wanisikie nikinena nawe na kila mara
waweke tumaini lao kwako.” Kisha Mose
akamwambia BWANA yale ambayo watu
walikuwa wamesema.
10 [i]Naye BWANA akamwambia Mose,
“Nenda kwa watu ukawaweke wakfu leo
na kesho. Waambie wafue nguo zao 11 [j]na
wawe tayari siku ya tatu, kwa sababu
siku hiyo, BWANA atashuka juu ya mlima
Sinai machoni pa watu wote. 12 Weka
mipaka kuzunguka mlima kwa ajili ya
watu, uwaambie, ‘Mwe waangalifu, msije
mkapanda mlimani au kuugusa. Yeyote
atakayeugusa mlima hakika atauawa.
13 [k]Hakika atapigwa mawe au kupigwa
mishale; mkono wa mtu hautamgusa. Akiwa
mwanadamu au mnyama, hataruhusiwa
kuishi.’ Ila tu wakati baragumu
itakapopigwa kwa mfululizo, ndipo watu
wote watakapopanda mlimani.”
14 [l]Baada ya Mose kushuka kutoka
mlimani akawaendea watu na kuwaweka
wakfu, wakafua nguo zao. 15 [m]Kisha
akawaambia watu, “Jitayarisheni kwa
ajili ya siku ya tatu. Mwanaume yeyote
asimkaribie mwanamke.”
16 [n]Asubuhi ya siku ya tatu kulikuwa na
ngurumo na radi pamoja na wingu nene
juu ya mlima na mlio mkubwa sana wa
tarumbeta. Kila mmoja aliyekuwa kambini
akatetemeka. 17 [o]Kisha Mose akawaongoza
watu kutoka kambini kukutana na Mungu,
nao wakasimama chini ya mlima. 18 [p]Mlima
Sinai ulikuwa umefunikwa na moshi, kwa
sababu BWANA alishuka juu yake katika

[a]**19:2** Kut 17:1; 36:1; Kum 5:2-4
[b]**19:3** Kut 20:21; 3:4; 25:22; Mdo 7:38
[c]**19:4** Kum 29:2; Yos 24:7; Kum 32:11; Za 103:5; Isa 40:31; Yer 4:13; 48:40; Ufu 12:14; Kum 33:12; Isa 31:5; Eze 16:6
[d]**19:5** Kut 15:26; Kum 6:3; Za 78:10; Yer 7:23; Mwa 17:9; Kut 3:1; 8:22; 34:9; Kum 1:8; Tit 2:14; Kut 9:29; 1Kor 10:26
[e]**19:6** Isa 61:6; 66; 21; 1Pet 2:5; Mwa 18:19; Law 11:45; Kum 4:27; 7:6; 26:19; 28:9; 29:13; 33:3; Isa 4:3; 62:12; Yer 2:3; Amo 3:2
[f]**19:7** Kut 18:12; Law 4:15; 9:1; Hes 16:25; Kut 4:30; Isa 8:10
[g]**19:8** Kut 24:3-7; Kum 5:27; 26:17
[h]**19:9** Kut 20:21; 24:15-16; 33:9; 34:5; Kum 4:11; 2Sam 22:10-12; 2Nya 6:1; Kut 4:5; Za 18:11; 97:2; 99:7; Mt 17:5; Kum 4:12, 36; Yn 12:29-30
[i]**19:10** Law 11:44; Hes 11:18; Isa 16:5; Yoe 2:16; Ebr 10:22; Mwa 35:2; Ufu 22:14
[j]**19:11** Mwa 11:5; Kut 3:1; 24:16; 31:18; 34:2-4, 29-32; Law 7:38; 26:46; 27:34; Hes 3:1; Dan 10:5; Neh 9:13; Gal 4:24-25
[k]**19:13** Ebr 12:20; Yos 6:4; 1Nya 15:28; Za 81:3; 98:6; Kut 34:3
[l]**19:14** Mwa 35:2
[m]**19:15** 1Sam 21:4; 1Kor 7:5
[n]**19:16** 1Sam 2:10; Isa 29:6; Ebr 12:18-19; Ufu 4:1; Mwa 3:10; 1Sam 13:7; 14:15; 28:5; Za 99:1; Ebr 12:21
[o]**19:17** Kum 4:11
[p]**19:18** Kut 20:18; Za 104:32; Isa 6:4; Ufu 15:8; Kut 3:2; 24:17; Law 9:24; Kum 4:11, 24, 33; 5:4; 9:3; 1Fal 18:24, 38; 1Nya 21:26; 2Nya 7:1; Za 18:8; Ebr 12:18; Mwa 19:28; Ufu 9:2; Amu 5:5; 2Sam 22:8; Za 68:8; Isa 2:19; 5:25; 41:15; 64:1; Yer 4:24; 10:10; Mik 1:4; Nah 1:5; Hab 3:6-10; Hag 2:6

moto. Moshi wa moto huo ulipanda
juu kama moshi kutoka kwenye tanuru
kubwa na mlima wote ukatetemeka kwa
nguvu nyingi, [19] [a]nayo sauti ya tarumbeta
ikawa kubwa zaidi na zaidi. Kisha Mose
akazungumza na sauti ya BWANA ikamjibu.
[20] BWANA akashuka juu ya Mlima Sinai na
akamwita Mose apande juu mlimani. Kwa
hiyo Mose akapanda juu, [21] [b]naye BWANA
akamwambia Mose, "Shuka ukawaonye
watu ili wasijipenyeze kutafuta kumwona
BWANA na wengi wao wakafa. [22] [c]Hata
makuhani, watakaomkaribia BWANA ni
lazima wajiweke wakfu, la sivyo BWANA
atawaadhibu."
[23] Mose akamwambia BWANA, "Watu
hawawezi kupanda mlima Sinai kwa sababu
wewe mwenyewe ulituonya ukisema,
'Wekeni mipaka kuuzunguka mlima na
kuutenga kama patakatifu.' "
[24] [d]BWANA akajibu, "Shuka ukamlete
Aroni pamoja nawe. Lakini makuhani
pamoja na watu wasije wakalazimisha kuja
kwa BWANA, nisije nikawaadhibu."
[25] Basi Mose akashuka kwa watu na
kuwaambia lile aliloambiwa.

*Amri Kumi*

**(Kumbukumbu 5:1-21)**

20 [e]Ndipo Mungu akasema maneno haya
yote:

[2] [f]"Mimi ndimi BWANA Mungu
wako, niliyekutoa Misri, kutoka
nchi ya utumwa.
[3] [g]Usiwe na miungu mingine ila mimi.
[4] [h]Usijitengenezee sanamu katika
umbo la kitu chochote kilicho
juu mbinguni, au duniani chini,
au ndani ya maji. [5] [i]Usivisujudie
wala kuviabudu; kwa kuwa Mimi,
BWANA Mungu wako, ni Mungu
mwenye wivu, ninayewaadhibu
watoto kwa ajili ya dhambi za
baba zao hadi kizazi cha tatu na
cha nne cha wanichukiao, [6] [j]lakini
ninaonyesha upendo kwa maelfu
ya vizazi vya wale wanipendao na
kuzishika amri zangu.
[7] [k]Usilitaje bure jina la BWANA Mungu
wako, kwa kuwa BWANA hataacha
kumhesabia hatia yeye alitajaye
jina lake bure.
[8] [l]Ikumbuke siku ya Sabato, uitakase.
[9] [m]Kwa siku sita utafanya kazi
na kutenda shughuli zako zote,
[10] [n]lakini siku ya saba ni Sabato
kwa BWANA Mungu wako. Siku
hiyo hutafanya kazi yoyote, wewe,
wala mwanao au binti yako, wala
mtumishi wako wa kiume au wa
kike, wala wanyama wako, wala
mgeni aliye ndani ya malango
yako. [11] [o]Kwa kuwa kwa siku sita,
BWANA aliumba mbingu na nchi,
bahari na vyote vilivyomo, lakini
akapumzika siku ya saba. Kwa

[a]**19:19** Kum 4:33; Neh 9:13; Za 81:7
[b]**19:21** Kut 24:10-11; Hes 4:20; 1Sam 6:19
[c]**19:22** Law 10:3; 1Sam 16:5; 2Nya 29:5; Yoe 2:16; 2Sam 6:7
[d]**19:24** Kut 24:1, 9
[e]**20:1** Kum 10:4; Neh 9:13; Za 119:9; 147:19; Mal 4:4
[f]**20:2** Mwa 17:7; Kut 16:12; Law 19:2; 20:7; Isa 43:3; Eze 20:19; Mwa 15:7; Kut 6:6; 13:3; Eze 20:6
[g]**20:3** Kut 34:14; Kum 6:14; 13; 10; 2Fal 17:35; Za 44:20; 81:9; Yer 1:16; 7:6-9; 11:13; 19:4; 25:6
[h]**20:4** Kut 32:8; 34:17; Law 19:4; 26:1; Kum 4:15-23; 27:15; 2Sam 7:22; 1Fal 14:9; 2Fal 17:12; Isa 42:8; 44:9
[i]**20:5** Kut 23:13; Yos 23:7; Amu 6:10; 2Fal 17:35; Isa 44:15-19; 46:6; Kut 34:14; Kum 4:24; Yos 24:19; Mwa 9:25; Law 26:39; Kut 34:7; Hes 14:18; Yer 32:18
[j]**20:6** Kut 34:7; Hes 14:18; Kum 7:9; Yer 32:18; Lk 1:50; Rum 11:28
[k]**20:7** Kut 22:28; Law 18:21; 19:12; 22:2; 24:11, 16; Kum 6:13; 10:20; Ay 2:5-9; Za 63:11; Isa 8:21; Eze 20:39; 39:7; Mt 5:33
[l]**20:8** Kut 16:23; 31:13-16; 35:3; Law 19:3, 30; 26:2; Isa 56:2; Yer 17:21-27; Eze 22:8
[m]**20:9** Kut 23:12; 31:13-17; 34:21; 35:2-3; Law 23:3; Lk 13:14
[n]**20:10** Mwa 2:3; Kut 31:14; Law 23:38; Hes 28:9; Isa 56:2; Eze 20:12, 20
[o]**20:11** Mwa 1:3–2:1; 2:2; Kut 31:17; Eze 4:4

hiyo BWANA akaibariki siku ya
Sabato na kuifanya takatifu.
12 [a]Waheshimu baba yako na mama
yako, ili upate kuishi siku nyingi
katika nchi anayokupa BWANA
Mungu wako.
13 [b]Usiue.
14 [c]Usizini.
15 [d]Usiibe.
16 [e]Usimshuhudie jirani yako uongo.
17 [f]Usiitamani nyumba ya jirani yako.
Usimtamani mke wa jirani yako,
wala mtumishi wake wa kiume au
wa kike, wala ng'ombe wake au
punda wake, wala chochote kile
alicho nacho jirani yako."

*Watu Wanaogopa*

**(Kumbukumbu 5:22-33)**

18 [g]Watu walipoona ngurumo na radi, na
kusikia mlio wa tarumbeta, na kuuona mlima
katika moshi, walitetemeka kwa woga.
Wakasimama mbali 19 [h]na wakamwambia
Mose, "Sema nasi wewe mwenyewe, nasi
tutakusikiliza. Lakini usimwache Mungu
aseme nasi, la sivyo tutakufa."
20 [i]Mose akawaambia watu, "Msiogope!
Mungu amekuja kuwajaribu, ili kwamba
hofu ya Mungu iwakalie, msitende dhambi."
21 [j]Watu wakabaki mbali, wakati Mose
alipolisogelea lile giza nene mahali pale
Mungu alipokuwa.

*Sanamu Na Madhabahu*

22 [k]Kisha BWANA akamwambia Mose,
"Waambie Waisraeli hivi: 'Mmejionea
wenyewe kwamba nimesema nanyi kutoka
mbinguni: 23 [l]Msijifanyizie miungu yoyote
na kuilinganisha nami, msijitengenezee
miungu ya fedha wala miungu ya dhahabu.
24 [m]" 'Utanitengenezea madhabahu
ya udongo, na juu yake utoe sadaka za
kuteketezwa kwa moto na sadaka za
amani, kondoo zako, mbuzi na ng'ombe
zako. Popote nitakapofanya Jina langu
liheshimiwe, nitakuja kwenu na kuwabariki.
25 [n]Ikiwa unanitengenezea madhabahu ya
mawe, usiijenge kwa mawe ya kuchonga,
maana mkitumia chombo cha kuchongea
mtaitia unajisi. 26 [o]Msitumie ngazi kupandia
kwenye madhabahu yangu, uchi wako usije
ukadhihirika kwa chini.'

*Watumishi Wa Kiebrania*

**(Kumbukumbu 15:12-18)**

21 [p]"Hizi ndizo sheria utakazoweka mbele
ya Waisraeli:

2 [q]"Kama ukimnunua mtumwa wa
Kiebrania, atakutumikia kwa miaka sita.
Lakini katika mwaka wa saba, atakuwa
huru naye atakwenda zake pasipo kulipa
chochote. 3 Kama akija peke yake,

[a]**20:12** Kum 5:16; Mt 15:4; 19:19; Mk 7:10; 10:19; Lk 18:20; Efe 6:2; Kum 6:2; Efe 6:3; Kum 11:9; 25:15; Yer 35:7
[b]**20:13** Mwa 4:23; Mt 5:21; 19:18; Lk 18:20; Rum 13:8-9; Yak 2:11
[c]**20:14** Law 18:20; 20:10; Hes 5:12, 13, 29; Mit 6:29-32; Mt 5:27; 19:18; Mk 10:19; Lk 18:20; Rum 13:9; Yak 2:11
[d]**20:15** Law 19:11-13; Eze 18:7; Mt 19:18; Mk 10:19; Lk 18:20; Rum 13:9
[e]**20:16** Law 19:11; Yer 9:3-5; Kut 23:1, 7; Law 19:18; Za 50:20; 101:5; 119:29; Mt 19:18; Mk 10:19; Lk 3:14; 18:20
[f]**20:17** Lk 12:15; Rum 7:7; 13:9; Efe 5:3; Ebr 13:5
[g]**20:18** Kut 19:16-19; Kum 4:36; Isa 58:1; Yer 6:17; Eze 33:3; Ebr 12:1-19; Ufu 1:10; Kut 19:18; Mwa 3:10; Kut 14:31; 19:16
[h]**20:19** Ay 37:4-5; 40:9; Za 29:3-4; Kum 5:23-27; 18:16; Gal 3:19
[i]**20:20** Mwa 15:1; 22:1; Kum 4:10; 6:2; 10:12; Za 111:10; 128:1; Mit 1:7; Mhu 12:13; Isa 8:13; Ay 1:8; 2:3; 28:28; Mit 3:7; 8:13; 14:16; 16:6
[j]**20:21** Kut 19:9; Kum 5:22; Za 81:8; 68:4; 97:2; Isa 19:1
[k]**20:22** Kum 5:24-26; Neh 9:13
[l]**20:23** Kut 22:20; 32:4, 8; 34:17; Kum 29:17-18; Neh 9:18
[m]**20:24** Kut 27:1; 40:29; Hes 16:38; Kum 27:5; Yos 8:30; 2Fal 16:14; 2Nya 4:1; Eze 43:13; Mwa 8:20; Kut 18:12; Kum 12:5; 16:6, 11; 26:2; 1Fal 9:3; 2Fal 21:4-7; 2Nya 6:6; 12:13; Ezr 6:12; Mwa 12:2; 22:17
[n]**20:25** Yos 8:31; 1Fal 6:7
[o]**20:26** Eze 43:17
[p]**21:1** Kut 24:3; 34:32; Kum 4:14; 6:1
[q]**21:2** Kut 22:3; Yer 34:8, 14; Law 25:39; Kum 15:12

atakwenda huru peke yake, lakini kama
akija na mke, ataondoka pamoja naye.
4 [a]Kama bwana wake alimpatia mke naye
akamzalia wana au binti, mwanamke
pamoja na watoto wake watakuwa mali
ya bwana wake na huyo mwanaume
ataondoka peke yake.
5 [b]“Lakini kama mtumishi akisema,
‘Ninampenda bwana wangu, mke wangu
pamoja na watoto na sitaki kuwa huru,’
6 [c]ndipo bwana wake atakapolazimika
kumpeleka mbele ya waamuzi. Kisha
atampeleka kwenye mlango au kizingiti
na kutoboa sikio lake kwa shazia. Naye
atamtumikia bwana wake maisha yake
yote.
7 [d]“Kama mtu akimuuza binti yake
kuwa mtumwa, hataachwa huru kama
watumwa wa kiume waachiwavyo. 8 Kama
hakumpendeza bwana wake aliyemchagua,
huyo bwana atamwacha akombolewe.
Hatakuwa na haki ya kumuuza kwa
wageni, kwa sababu huyo bwana atakuwa
amekosa uaminifu. 9 Kama akimchagua
aolewe na mwanawe, ni lazima ampe haki
za kuwa binti yake. 10 [e]Ikiwa huyo mwana
aliyeozwa mtumwa mwanamke ataoa
mwanamke mwingine, ni lazima aendelee
kumtosheleza huyo mke wa kwanza kwa
chakula, mavazi na haki zote za ndoa.
11 Iwapo hatamtosheleza kwa mambo hayo
matatu, huyo mke wa kwanza ataondoka
na kuwa huru bila malipo yoyote ya fedha.

*Majeraha Ya Mwilini*

12 [f]“Yeyote ampigaye mtu na kumuua ni
lazima auawe hakika. 13 [g]Hata hivyo, kama
hakumuua kwa makusudi, lakini Mungu
akaruhusu itendeke, basi atakimbilia
mahali nitakapomchagulia. 14 [h]Lakini kama
mtu akipanga na kumuua mwingine kwa
makusudi, mwondoe katika madhabahu
yangu na kumuua.
15 “Yeyote amshambuliaye baba yake au
mama yake ni lazima auawe.
16 [i]“Yeyote amtekaye nyara mwingine
akamuuza au akamweka kwake,
akikamatwa ni lazima auawe.
17 [j]“Yeyote atakayemlaani baba yake au
mama yake ni lazima auawe.
18 “Kama watu wakigombana na mmoja
akimpiga mwingine kwa jiwe au kwa
ngumi yake na hakufa bali akaugua na
kulala kitandani, 19 [k]yule aliyempiga
ngumi hatahesabiwa kuwa na hatia kama
mwenzake ataamka na kujikongoja kwa
fimbo yake, lakini hata hivyo, ni lazima
amlipe fidia ya muda wake aliopoteza na
awajibike mpaka apone kabisa.
20 [l]“Kama mtu akimpiga mtumwa wake
wa kiume au wa kike kwa fimbo na mtumwa
huyo akafa papo hapo, ni lazima aadhibiwe
21 [m]lakini ikiwa mtumwa ataamka baada
ya siku moja au mbili, hataadhibiwa, kwa
sababu yule mtumwa ni mali yake.
22 [n]“Ikiwa watu wawili wanapigana na
wakamuumiza mwanamke mjamzito,
naye akazaa kabla ya wakati lakini
hakuna majeraha makubwa, mhalifu
atatozwa mali kiasi cha madai ya mume
wa yule mwanamke, na jinsi mahakama
itakavyoamua. 23 [o]Lakini kukiwa na jeraha
kubwa, ni lazima ulipe uhai kwa uhai,
24 [p]jicho kwa jicho, jino kwa jino, mkono
kwa mkono, mguu kwa mguu, 25 kuchomwa
moto kwa kuchomwa moto, jeraha kwa
jeraha, mchubuko kwa mchubuko.

[a]**21:4** Law 25:44
[b]**21:5** Kum 15:16
[c]**21:6** Kut 22:8-9; Kum 17:9; 19:17; 21:5; Za 40:6; Ay 39:9; 41:4
[d]**21:7** Neh 5:5
[e]**21:10** 1Kor 7:3-5
[f]**21:12** Mwa 4:14, 23; Kut 31:15; Law 20:9-10; 24:16; 27:29; Hes 1:51; 35:16, 30-31; Kum 13:5; 19:11; 22:22; 27:16; Ay 31:11; Mit 20:20; Mt 26:52; Mwa 9:6
[g]**21:13** Hes 35:10-34; Kum 4:42; 19:2-13; Yos 20:9; 1Sam 24:4; 10:18; Yos 20:2
[h]**21:14** Mwa 4:8; Hes 35:20; 2Sam 3:27; 20:10; Ebr 10:26; Kum 19:11-12; 1Fal 2:28-34
[i]**21:16** Mwa 37:28; Kut 22:4; Kum 24:7
[j]**21:17** Kum 5:16; Mt 15:4; Mk 7:10; Law 20:9; Mit 20:20
[k]**21:19** 2Sam 3:29
[l]**21:20** Law 25:43; Efe 6:9
[m]**21:21** Law 25:44-46
[n]**21:22** Kum 22:18, 19
[o]**21:23** Law 24:19; Kum 19:21
[p]**21:24** Kut 21:23; Mt 5:38; Kum 19:21; Mt 5:38; 7:2; Law 24:20

26 [a]“Ikiwa mtu atampiga mtumwa
mwanaume au mwanamke kwenye jicho
na kuliharibu, ni lazima amwache huru
yule mtumwa kama fidia ya hilo jicho.
27 Kama akimvunja jino mtumwa wa kiume
au wa kike, ni lazima amwache huru huyo
mtumwa kwa kufidia hilo jino.

28 [b]“Kama fahali akimuua mwanaume
au mwanamke kwa kumpiga kwa pembe,
fahali huyo ni lazima auawe kwa kupigwa
mawe, na nyama yake haitaliwa. Lakini
mwenye fahali huyo hatawajibika. 29 Lakini
hata hivyo, ikiwa huyo fahali amekuwa na
tabia ya kupiga kwa pembe, na mwenyewe
ameonywa na hakutaka kumfungia naye
akamuua mwanaume au mwanamke,
huyo fahali ni lazima auawe kwa mawe na
mwenye fahali pia auawe. 30 [c]Lakini ikiwa
malipo yatatakiwa kwake, basi anaweza
kulipa kinachodaiwa ili kuukomboa uhai
wake. 31 Sheria hii pia itatumika ikiwa
fahali atampiga kwa pembe mwana au binti.
32 [d]Ikiwa fahali atampiga mtumwa wa kike
au wa kiume, mwenye fahali atalipa shekeli
thelathini[e] za fedha kwa bwana mwenye
mtumwa, na fahali ni lazima auawe kwa
mawe.

33 [f]“Kama mtu akiacha shimo wazi,
ama akachimba shimo kisha asilifukie,
na ng’ombe au punda akatumbukia ndani
yake, 34 mwenye shimo ni lazima alipe
hasara iliyotokea; ni lazima amlipe mwenye
mnyama. Mnyama aliyekufa atakuwa wake.

35 “Kama fahali wa mtu fulani atamuumiza
fahali wa mtu mwingine na akafa,
watamuuza yule aliye hai na wagawane
sawa fedha pamoja na mnyama aliyekufa.
36 Hata hivyo, kama ikifahamika kwamba
fahali huyo alikuwa na tabia ya kupiga
kwa pembe na mwenyewe hakumfunga,
ni lazima mwenye fahali alipe mnyama kwa
mnyama, na mnyama aliyekufa atakuwa
wake.

[a]**21:26** Kol 4:1
[b]**21:28** Mwa 9:5
[c]**21:30** Hes 35:21
[d]**21:32** Mwa 37:28; Mt 26:15; 27:3, 9; Zek 11:12, 13; Flp 2:7
[e]32 Shekeli 30 ni sawa na gramu 300.
[f]**21:33** Lk 14:5

*Ulinzi Wa Mali*

22 [g]“Kama mtu akiiba maksai au kondoo
na kumchinja au kumuuza, ni lazima
alipe ng’ombe watano badala ya maksai
mmoja na kondoo wanne badala ya kondoo
mmoja.

2 [h]“Kama mwizi akishikwa anavunja
nyumba akapigwa hata akafa, aliyemuua
hana hatia ya kumwaga damu; 3 [i]lakini jambo
hilo likitokea wakati jua limechomoza,
huyo mtu atakuwa na hatia ya kumwaga
damu.

“Mwizi huyo sharti alipe, lakini kama
hana kitu, lazima auzwe ili alipe kwa ajili
ya wizi wake.

4 [j]“Kama mnyama aliyeibwa akikutwa
hai mikononi mwake, ikiwa ni maksai au
punda au kondoo, lazima alipe mara mbili.

5 “Kama mtu akichunga mifugo yake
katika shamba au shamba la mizabibu, na
akawaachia wajilishe katika shamba la mtu
mwingine, ni lazima alipe vitu bora kutoka
kwenye shamba lake mwenyewe au kutoka
shamba lake la mizabibu.

6 [k]“Kama moto ukiwaka na kuenea
kwenye vichaka vya miiba na kuteketeza
miganda ya nafaka au nafaka ambayo
haijavunwa, au kuteketeza shamba lote,
mtu yule aliyewasha moto lazima alipe.

7 [l]“Kama mtu akimpa jirani yake fedha
au mali nyingine amtunzie, na kama
vikiibwa kutoka nyumba ya huyo jirani,
kama mwizi atashikwa, lazima alipe mara
mbili. 8 [m]Lakini mwizi asipopatikana,
mwenye nyumba atafika mbele ya waamuzi
ili kuthibitisha kuwa hakuchukua mali ya
mwenzake. 9 [n]Pakiwepo jambo lolote la
mali isiyo halali, ikiwa ni maksai, punda,
kondoo, mavazi, ama mali yoyote iliyopotea

[g]**22:1** Law 6:1-7; 2Sam 12:6; Mit 6:31; Lk 19:8
[h]**22:2** Ay 24:16; Yer 2:34; Hos 7:1; Mt 6:19-20; 24:43; Hes 35:27; Kut 20:15; Law 19:11; Kum 5:19; Lk 18:20; Rum 13:9; Efe 4:28; 1Pet 4:15
[i]**22:3** Kut 21:2; Mt 18:25
[j]**22:4** 1Sam 12:5; Mwa 43:12; Kut 21:16; Mit 6:31
[k]**22:6** Amu 15:5
[l]**22:7** Law 6:2; Mwa 43:12
[m]**22:8** Kut 21:6; Kum 17:8-9
[n]**22:9** Kum 25:1

ambayo fulani atasema, ‘Hii ni mali yangu,’
pande zote mbili wataleta mashauri yao
mbele ya waamuzi. Yule ambaye waamuzi
watamwona kuwa na hatia atamlipa jirani
yake mara mbili.
10 “Kama mtu akimpa jirani yake punda,
ng’ombe, kondoo au mnyama mwingine
yeyote amtunzie, akifa au akijeruhiwa
au akichukuliwa wakati haonekani na
mtu yeyote, 11 [a]jambo hili kati yao wawili
litaamuliwa kwa kuapa kiapo mbele za
BWANA, kwamba huyo jirani hakuhusika
na wizi wa mali ya jirani yake. Mwenye
mali itampasa akubali jambo hili, na
hakuna malipo yatakayohitajika. 12 Lakini
kama mnyama aliibwa kwa jirani, itampasa
amlipe mwenye mnyama. 13 [b]Kama
ameraruliwa na mnyama pori, ataleta
mabaki ya mnyama kama ushahidi, naye
hatadaiwa kulipa mnyama aliyeraruliwa.
14 “Kama mtu akimwazima mnyama
kutoka kwa jirani yake, na kama akiumia au
akafa na mwenye mnyama hayupo, lazima
amlipe huyo mnyama. 15 [c]Lakini mwenye
mnyama akiwa angalipo na mnyama wake,
mwazimaji hatalazimika kumlipa. Kama
mnyama alikuwa amekodishwa, fedha
iliyolipwa kwa kukodisha inatosha kwa
kufidia hasara.

*Uwajibikaji Wa Kijamii*

16 [d]“Kama mtu akimshawishi bikira
ambaye hajaposwa na akilala naye, lazima
alipe mahari, kisha atamwoa msichana
huyo. 17 Baba wa msichana akikataa
katakata kumpa huyo mtu huyo msichana
wake, bado ni lazima huyo mtu atalipa
mahari kama inavyostahili malipo ya
ubikira.
18 [e]“Usiruhusu mwanamke mchawi aishi.
19 [f]“Mtu yeyote aziniye na mnyama
lazima auawe.
20 [g]“Mtu awaye yote anayemtolea mungu
mwingine dhabihu isipokuwa BWANA,
lazima aangamizwe.
21 “Usimtendee mgeni vibaya au
kumwonea, kwa kuwa nanyi mlikuwa
wageni huko Misri.
22 [h]“Usimdhulumu mjane wala yatima.
23 [i]Kama ukifanya hivyo nao wakinililia,
hakika nitasikia kilio chao. 24 [j]Hasira yangu
itawaka, nami nitawaua kwa upanga, wake
zenu watakuwa wajane na watoto wenu
watakuwa yatima.
25 [k]“Kama ukimkopesha mmojawapo
wa watu wangu fedha ambaye ni mhitaji,
usiwe kama mtu mkopesha fedha; usimtoze
riba. 26 [l]Kama ukichukua vazi la jirani kama
rehani, ulirudishe kwake kabla jua kuzama,
27 [m]kwa kuwa vazi lake ndilo pekee alilo
nalo la kumfunika mwili wake. Ni nini
kingine atajifunika nacho? Atakaponililia,
nitasikia, kwa kuwa nina huruma.
28 [n]“Usimkufuru Mungu au kumlaani
mtawala wa watu wako.
29 [o]“Usiache kutoa sadaka kutoka ghala
lako au mapipa yako.
“Lazima unipe mzaliwa wa kwanza wa
wana wako. 30 [p]Ufanye vivyo hivyo kwa
ng’ombe wako na kwa kondoo wako.

[a]**22:11** Law 6:3; 1Fal 8:31; 2Nya 6:22; Ebr 6:16
[b]**22:13** Mwa 31:39
[c]**22:15** Law 19:13; Ay 17:5
[d]**22:16** Kum 22:28; Mwa 34:12
[e]**22:18** Kut 7:11; Law 19:26, 31; 20:27; Kum 18:17; 1Sam 28:3; 2Nya 33:6; Isa 57:3
[f]**22:19** Law 18:23; 20:15; Kum 27:21
[g]**22:20** Kut 20:23; 22:21
[h]**22:22** Kum 10:18; 24:6, 10-17; Ay 22:6-9; 24:3; 21; Za 68:5; 146:9; Mit 23:10; Isa 1:17; Yer 7:5-6; 21:12; 22:3; Eze 18:5-12; Zek 7:9-10; Mal 3:5; Yak 1:27
[i]**22:23** Lk 18:7; Kum 10:18; 15:9; 24:15; Ay 34:28; 35:9; Za 10:14-17; 12:5; 18:6; Yak 5:4
[j]**22:24** Za 10:9; 69:24; Mao 5:3
[k]**22:25** Law 25:35-37; Kum 15:7-11; 23:20; Neh 5:7-10; Za 15:5; Eze 18:8
[l]**22:26** Mit 20:16; Eze 33:15; Amo 2:8
[m]**22:27** Kum 24:13, 17; Ay 22:6; 24:7; 29:11; 31:19-20; Eze 18:12, 16; Kut 34:6; Kum 4:31; 2Nya 30:9; Neh 9:17; Za 99:8; 103:8; 116:5; 145:8; Yoe 2:13; Yon 4:2
[n]**22:28** Kut 20:7; 2Sam 16:5, 9; 1Sam 19:21; 1Fal 21:10; 2Fal 2:23; Za 102; 8; Mhu 10:20; Mdo 23:5
[o]**22:29** Kut 23:15-19; 34:20-26; Law 19:24; 23:10; Hes 18:13; 28:26; Kum 18:4; 26:2, 10; 1Sam 6:3; Neh 10:35; Mit 3:9; Mal 3:10; Kut 13:2; Hes 8:16-17; Lk 2:23
[p]**22:30** Kut 34:19; Kum 15:19; Law 12:3; 22:27; Mwa 17:12

Waache wakae na mama zao kwa siku saba,
lakini siku ya nane unipe.
31 [a]“Ninyi mtakuwa watu wangu
watakatifu. Kwa hiyo msile nyama ya
mnyama aliyeraruliwa na wanyama pori;
mtupieni mbwa.

*Sheria Za Haki Na Rehema*

23 [b]“Usieneze habari za uongo. Usimsaidie
mtu mwovu kwa kuwa shahidi
mwenye nia ya kudhuru wengine.
2 [c]“Usifuate umati wa watu katika kutenda
mabaya. Unapotoa ushahidi kwenye
mashtaka, usipotoshe haki ukijumuika na
umati wa watu, 3 [d]nawe usimpendelee mtu
maskini katika mashtaka yake.
4 “Kama ukikutana na maksai au
punda wa adui yako anapotea, hakikisha
umemrudisha kwake. 5 [e]Ukiona punda wa
mtu anayekuchukia ameanguka na mzigo
wake, usimwache hapo alipoangukia;
hakikisha kuwa umemsaidia.
6 [f]“Usiwanyime haki watu wako walio
maskini katika mashtaka yao. 7 [g]Ujiepushe
na mashtaka ya uongo, wala usimuue mtu
asiye na hatia au mtu mwaminifu, kwa
maana sitamhesabia hana hatia yeye aliye
na hatia.
8 [h]“Usipokee rushwa, kwa kuwa rushwa
hupofusha wale waonao, na kupinda
maneno ya wenye haki.
9 [i]“Usimwonee mgeni; ninyi wenyewe
mnajua jinsi mgeni anavyojisikia, kwa
sababu mlikuwa wageni Misri.

*Sheria Za Sabato*

10 “Kwa muda wa miaka sita mtapanda
mashamba yenu na kuvuna mazao, 11 [j]lakini
katika mwaka wa saba usiilime ardhi wala
kuitumia, ili watu walio maskini miongoni
mwenu waweze kupata chakula kutoka
kwenye hayo mashamba, nao wanyama
pori wapate chakula kwa yale mabaki
watakayobakiza. Utafanya hivyo katika
shamba lako la mizabibu na la mizeituni.
12 [k]“Kwa siku sita fanya kazi zako, lakini
siku ya saba usifanye kazi, ili maksai wako
na punda wako wapate kupumzika, naye
mtumwa aliyezaliwa nyumbani mwako,
pamoja na mgeni, wapate kustarehe.
13 [l]“Uzingatie kutenda kila kitu
nilichokuambia. Usiombe kwa majina ya
miungu mingine, wala usiyaruhusu kusikika
kinywani mwako.

*Sikukuu Tatu Za Mwaka*

**(Kutoka 34:18-26; Kumbukumbu 16:1-17)**

14 [m]“Mara tatu kwa mwaka utanifanyia
sikukuu.
15 [n]“Utaadhimisha Sikukuu ya Mikate
Isiyotiwa Chachu; kwa siku saba
utakula mikate isiyotiwa chachu kama
nilivyokuagiza. Fanya jambo hili kwa
wakati uliopangwa katika mwezi wa Abibu,
ndio mwezi wa nne, kwa sababu katika
mwezi huo ulitoka Misri.
“Mtu yeyote asije mbele yangu mikono
mitupu.

---

[a]**22:31** Kut 19:6; Law 19:2; 22:31; Ezr 9:2; Law 7:24; 17:15; 22:8; Kum 14:21; Eze 4:14; 44:31
[b]**23:1** Mwa 36:7; Mt 19:18; Lk 3:14; Kut 20:16; Kum 5:20; 19:16-21; Za 27:12; 35:11; Mit 19:5; Mdo 6:11
[c]**23:2** Law 19:15, 33; Kum 1:17; 27:19; 1Sam 8:3; Kum 24:17; 16:19; Ay 31:34
[d]**23:3** Rum 12:20; Law 6:2-3; 19:11; Kum 22:1-2
[e]**23:5** Kum 22:4
[f]**23:6** Kum 23:16; Mit 22:22
[g]**23:7** Kut 20:16; Efe 4:24-25; Mt 27:4; Mwa 18:23; Kut 34:7; Kum 19:18; 25:1
[h]**23:8** Kut 18:21; Law 9:15; Kum 10:17; 27:25; Ay 15:34; 36:18; Za 26:10; Mit 6:35; 15:27; 17:8; Isa 1:23; 5:23; Mik 3:11; 7:3
[i]**23:9** Kut 22:21; Law 19:33-34; Eze 22:7
[j]**23:11** Law 25:1-7; Neh 10:31
[k]**23:12** Kut 20:9; Lk 13:14; Mwa 2:2-3
[l]**23:13** Kum 4:9, 23; 1Tim 4:16; Kum 12:3; Yos 23:7; Za 16:4; Zek 13:2; Kum 18:20; Hos 2:17
[m]**23:14** Kut 12:14; 34:23-24; Kum 16:16; 1Fal 9:25; 2Nya 8:13; Eze 46:9
[n]**23:15** Kut 12:17; Mt 26:17; Lk 22:1; Mdo 12:3; Kut 12:2; 22:29

16 [a]“Utaadhimisha Sikukuu ya Mavuno
kwa malimbuko ya mazao yako uliyopanda
katika shamba lako.
“Utaadhimisha Sikukuu ya Kukusanya
mavuno mwishoni mwa mwaka,
unapokusanya mavuno yako toka shambani.
17 “Mara tatu kwa mwaka wanaume wote
watakuja mbele za BWANA Mwenyezi.
18 [b]“Msitoe damu ya dhabihu kwangu
pamoja na kitu chochote kilicho na chachu.
“Mafuta ya mnyama wa sadaka ya
sikukuu yangu yasibakizwe mpaka asubuhi.
19 “Utaleta malimbuko bora ya ardhi yako
katika nyumba ya BWANA Mungu wako.
“Usimchemshe mwana-mbuzi katika
maziwa ya mama yake.

### *Malaika Wa Mungu Kuandaa Njia*

20 [c]“Tazama, ninamtuma malaika
akutangulie mbele yako akulinde njiani
na kukuleta mpaka mahali nilipoandaa.
21 [d]Mtamtii na kusikiliza kile anachokisema.
Usiasi dhidi yake; hatakusamehe uasi wako,
kwa maana Jina langu limo ndani yake.
22 [e]Kama ukitii kweli kweli kile asemacho na
kufanya yote nisemayo, nitakuwa adui wa
adui zako, na nitawapinga wale wakupingao.
23 [f]Malaika wangu atatangulia mbele yako
na kukuleta katika nchi ya Waamori,
Wahiti, Waperizi, Wakanaani, Wahivi
na Wayebusi, nami nitawafutilia mbali.
24 [g]Usiisujudie miungu yao, au kuiabudu,
wala kufuata desturi yao. Utayabomoa
kabisa na kuvunjavunja mawe yao ya ibada
vipande vipande. 25 [h]Utamwabudu BWANA
Mungu wako, na baraka zake zitakuwa
juu ya vyakula vyako na maji yako. Nami
nitaondoa maradhi miongoni mwako,
26 [i]na hakuna atakayeharibu mimba wala
atakayekuwa tasa katika nchi yako. Nami
nitakupa maisha makamilifu.
27 [j]“Nitapeleka utisho wangu mbele yako
na kufadhaisha kila taifa utakalolifikia.
Nitafanya adui zako wote wakupe
kisogo na kukimbia. 28 [k]Nitatanguliza
manyigu mbele yako kuwafukuza Wahivi,
Wakanaani na Wahiti waondoke njiani
mwako. 29 [l]Lakini sitawafukuza kwa mara
moja, kwa sababu nchi itabaki ukiwa
na wanyama pori watakuwa wengi mno
kwako. 30 [m]Nitawafukuza kidogo kidogo
mbele yako, mpaka uwe umeongezeka kiasi
cha kutosha kuimiliki nchi.
31 [n]“Nitaweka mipaka ya nchi yako kuanzia
Bahari ya Shamu hadi Bahari ya Wafilisti, na
kuanzia jangwani hadi Mto Frati. Nitawatia
watu wanaoishi katika nchi hizo mikononi
mwako, nawe utawafukuza watoke mbele
yako. 32 [o]Usifanye agano lolote nao wala na
miungu yao. 33 [p]Usiwaache waishi katika
nchi yako, la sivyo watakusababisha utende
dhambi dhidi yangu, kwa sababu ibada ya
miungu yao hakika itakuwa mtego kwako.”

---

[a]**23:16** Law 23:15-21; Hes 28:26; Kum 16:9; 2Nya 8:13; Kut 22:29; 34:22; Law 23:34, 42; Kum 16:16; 31:10; Ezr 3:4; Neh 8:14; Zek 14:16; Yer 40:10; Kum 16:13
[b]**23:18** Kut 34:25; Law 2:11; Kut 12:8
[c]**23:20** Mwa 16:7; Kut 15:17; 32:34
[d]**23:21** Kum 18:19; Yer 13:15; Kum 29:20; 2Fal 24:4; Mao 1:17; Hes 17:10; Kum 9:7; 31:27; Yos 24:19; Za 25:7; 78:8, 40; 106:33; 107; 11; 1Yn 5:16; Kut 3:15
[e]**23:22** Kut 15:26; Mwa 12:3; Isa 41:11; Yer 30:20
[f]**23:23** Hes 13:29; 21:21; Yos 3:10; 24:8-10; 24:8-11; Ezr 9:1
[g]**23:24** Kut 20:5; Law 18:3; 20:23; Kum 9:4; 12:30-31; Yer 10:2; Kut 34:13; Hes 33:52; Kum 7:5; 12:3; Amu 2:2; 2Fal 18:4; 23:14; Kum 16:22; 1Fal 14:23; 3:2; 10:26; 17:20; 2Nya 14:2-3; Isa 27:9
[h]**23:25** Mt 4:10; Law 26:3-13; Kum 7:12-15; 28:1-14; Kut 15:26
[i]**23:26** Law 26:3-4; Kum 7:14; 28:4; Mal 3:11; Mwa 15:15; Kum 4:1, 40; 21:12
[j]**23:27** Mwa 35:5; Kut 15:14; 14:24; Kum 7:23; 2Sam 22:41; Za 18:40; 21:12
[k]**23:28** Kum 7:20; Yos 24:12; Kut 33:2; 34:11, 24; Hes 13:29; Kum 4:38; 11:23; 18:12; Yos 3:10; 24:11; Za 78:55
[l]**23:29** Kum 7:22
[m]**23:30** Yos 23:5
[n]**23:31** Mwa 2:14; Kum 34:2; Ezr 4:20; Kum 7:24; 9:3; Yos 21:44; 24:12-18; Za 80:8
[o]**23:32** Mwa 26:28; Kut 34:12; Kum 7:2; Yos 9:7; Amu 2:2; 1Sam 11:1; 1Fal 15:19; 20:34; Eze 17:13
[p]**23:33** Kut 10:7; Za 106:36

*Agano Lathibitishwa*

24 [a]Kisha Mungu akamwambia Mose,
"Njooni huku juu kwa BWANA, wewe
na Aroni, Nadabu na Abihu, pamoja na
wazee sabini wa Israeli. Mniabudu kwa
mbali, 2 [b]lakini Mose peke yake ndiye
atakayemkaribia BWANA; wengine wasije
karibu. Nao watu wasije wakapanda pamoja
naye."
3 [c]Mose alipokwenda na kuwaambia
watu maneno yote na sheria zote za
BWANA, wakaitikia kwa sauti moja, "Kila
kitu alichosema BWANA tutakifanya."
4 [d]Ndipo Mose akaandika kila kitu BWANA
alichokuwa amesema.
Akaamka kesho yake asubuhi na mapema
na kujenga madhabahu chini ya mlima
na kusimamisha nguzo kumi na mbili
za mawe kuwakilisha makabila kumi na
mawili ya Israeli. 5 [e]Kisha akawatuma vijana
wanaume wa Kiisraeli, nao wakatoa sadaka
za kuteketezwa na dhabihu za mafahali
wachanga kuwa sadaka za amani kwa
BWANA. 6 [f]Mose akachukua nusu ya damu
ya wale wanyama na kuiweka kwenye
mabakuli na nusu nyingine akainyunyiza
juu ya madhabahu. 7 [g]Kisha akachukua kile
Kitabu cha Agano na kuwasomea watu. Nao
wakajibu, "Tutafanya kila kitu alichosema
BWANA, nasi tutatii."
8 [h]Ndipo Mose akachukua ile damu,
akawanyunyizia wale watu, akasema,
"Hii ni damu ya agano ambalo BWANA
amelifanya nanyi kufuatana na maneno
haya yote."
9 Mose na Aroni, Nadabu na Abihu,
pamoja na wazee sabini wa Israeli
wakapanda mlimani, 10 [i]nao wakamwona
Mungu wa Israeli. Chini ya miguu yake
kulikuwa na kitu kama sakafu ya mawe
ya yakuti samawi, iliyo safi kama anga
angavu. 11 [j]Lakini Mungu hakuinua mkono
wake dhidi ya hawa viongozi wa Waisraeli;
walimwona Mungu, nao wakala na kunywa.
12 [k]BWANA akamwambia Mose, "Panda
uje kwangu huku mlimani na ukae hapa,
nami nitakupa vibao vya mawe, vyenye
sheria na amri ambazo nimeziandika ziwe
mwongozo wao."
13 [l]Basi Mose akaondoka na Yoshua
mtumishi wake, naye Mose akapanda
juu kwenye mlima wa Mungu. 14 [m]Mose
akawaambia wazee wa Israeli, "Tungojeni
hapa mpaka tutakapowarudia. Aroni na
Huri wako pamoja nanyi, na kila aliye na
neno aweza kuwaendea wao."
15 [n]Mose alipopanda juu mlimani, wingu
liliufunika huo mlima, 16 [o]nao utukufu wa
BWANA ukatua juu ya Mlima Sinai. Kwa
muda wa siku sita wingu lilifunika mlima,
na siku ya saba BWANA akamwita Mose
kutoka katikati ya lile wingu. 17 [p]Kwa
Waisraeli utukufu wa BWANA ulionekana
kama moto uteketezao juu ya mlima.
18 [q]Kisha Mose akaingia ndani ya lile wingu
alivyokuwa akipanda mlimani. Naye akakaa
huko mlimani kwa muda wa siku arobaini,
usiku na mchana.

---

[a]**24:1** Kut 19:24; 6:23; Hes 11:16; Law 10:1-2
[b]**24:2** Hes 12:6-8
[c]**24:3** Kut 21:1; Gal 3:19; Kut 19:8; Yos 24:24; Kum 5:27
[d]**24:4** Kut 17:14; Mwa 8:20; 28:18; Kum 31:9; 27:2
[e]**24:5** Law 1:3; Mwa 31:54
[f]**24:6** Kut 14:15; 32:31; Za 99:6; Ebr 9:18; Law 1:11; 3:2, 8; 5:9; Mt 26:28
[g]**24:7** 2Fal 23:2, 21; Ebr 9:19; Kut 19:8; Yer 40:3; 42:6, 21; 43:2
[h]**24:8** Ebr 9:19; 1Pet 1:2; Law 26:3; Kum 5:2-3; Yos 24:25; 2Fal 11:17; Yer 11:4-8; 31:32; 34:13; Zek 9:11; Mt 26:28; Lk 22:20; Ebr 9:20
[i]**24:10** Mwa 16:13; Hes 12:6; Isa 6:1; Eze 8:3; 40:2; Yn 1:18; Ay 28:16; Isa 54:11; Ufu 4:3
[j]**24:11** Kut 3:6; 19:2; Eze 44:3; Mt 26:29; Mwa 32:30
[k]**24:12** Kut 31:18; 32:15-16; 34:1, 28, 29; Kum 4:13; 5:22; 8:3; 9:9-11; 2Kor 3:12
[l]**24:13** Kut 17:9; 3:1
[m]**24:14** Kut 17:10; 18:16
[n]**24:15** Kut 19:9; Mt 17:5
[o]**24:16** Kut 16:7; Law 9:23; Hes 14:10; 1Sam 4:21-22; Eze 8:4; 11:22; Kut 19:11; Za 99:7
[p]**24:17** Kut 15:7; 19:18; Ebr 12:18, 29
[q]**24:18** 1Fal 19:8; Mwa 7:4; Mt 4:2; Kut 34:28; Kum 9:9

*Sadaka Kwa Ajili Ya Maskani Ya Mungu*

**(Kutoka 35:4-9)**

25 [a]BWANA akamwambia Mose,
2 “Waambie Waisraeli waniletee
sadaka. Utapokea sadaka kwa niaba
yangu kutoka kwa kila mtu ambaye moyo
wake wapenda kutoa. 3 Hizi ndizo sadaka
utakazozipokea kutoka kwao: dhahabu,
fedha na shaba; 4 [b]nyuzi za rangi ya buluu,
za zambarau, za rangi nyekundu, pamoja
na kitani safi; singa za mbuzi; 5 [c]ngozi za
kondoo dume zilizopakwa rangi nyekundu,
na ngozi za pomboo;[d] mbao za mshita;
6 [e]mafuta ya zeituni kwa ajili ya taa; vikolezi
kwa ajili ya mafuta ya upako, pamoja na
uvumba wa harufu nzuri; 7 [f]na vito vya
shohamu na vito vingine vya thamani vya
kuweka kwenye kisibau na kile kifuko cha
kifuani.

8 [g]“Kisha uwaamuru wanitengenezee
mahali patakatifu, nami nitakaa miongoni
mwao. 9 [h]Tengeneza hema hili na vyombo
vyake vyote sawasawa na kielelezo
nitakachokuonyesha.

*Sanduku La Agano*

**(Kutoka 37:1-9)**

10 [i]“Nao watatengeneza Sanduku la
mbao za mshita, lenye urefu wa dhiraa
mbili na nusu,[j] upana wa dhiraa moja na
nusu,[k] na kimo cha dhiraa moja na nusu.
11 [l]Utalifunika hilo Sanduku kwa dhahabu
safi ndani na nje, na kulifanyia ukingo wa
dhahabu juu yake kulizunguka. 12 Utalisubu
kwa pete nne za dhahabu na kuzifungia
kwenye miguu yake minne, pete mbili kwa
upande mmoja na pete mbili kwa upande
mwingine. 13 [m]Kisha utatengeneza mipiko ya
mti wa mshita na kuzifunika kwa dhahabu.
14 [n]Utaiingiza hiyo mipiko kwenye zile pete
katika pande mbili za Sanduku ili kulibeba.
15 [o]Hiyo mipiko itabakia daima katika hizo
pete za hilo Sanduku; haitaondolewa.
16 [p]Kisha weka ndani ya hilo Sanduku ule
Ushuhuda nitakaokupa.

17 [q]“Tengeneza kifuniko cha upatanisho
cha dhahabu safi, chenye urefu wa dhiraa
mbili na nusu, na upana wa dhiraa moja
na nusu. 18 [r]Tengeneza makerubi wawili
wa dhahabu iliyofuliwa katika miisho
ya hicho kifuniko. 19 Tengeneza kerubi
mmoja kwenye mwisho mmoja, na kerubi
mwingine kwenye mwisho mwingine;
watengeneze makerubi hao wawe kitu
kimoja na hicho kifuniko katika miisho
hiyo miwili. 20 [s]Makerubi hao watakuwa
wametandaza mabawa kuelekea juu,
yakitia kivuli hicho kifuniko. Makerubi hao
wataelekeana, wakitazama hicho kifuniko.
21 [t]Weka huo Ushuhuda nitakaokupa ndani
ya hilo Sanduku la Agano, na uweke hicho

[a]**25:1** Kut 35:21, 29; 36:2; 2Fal 12:4; 1Nya 29:5, 9; 2Nya 24:10; 29:31; Ezr 2:68; Neh 7:70; 2Kor 8:11; 9:7

[b]**25:4** Kut 28:4-8

[c]**25:5** Hes 4:6-10; Kum 10:3

[d]5 *Pomboo* hapa ina maana ya mnyama mwenye ngozi laini aishiye kwenye milima yenye misitu, au pengine nguva au sili.

[e]**25:6** Kut 27:20; 30:22-32; 35:28; 39:37; Hes 4:16; Kut 30:11; Law 16:12; Hes 7:14; 2Nya 13:11

[f]**25:7** Kut 28:4-14; 29:5; Amu 8:27; Hos 3:4; Law 8:8; Kut 28:15-30

[g]**25:8** Kut 36:1-5; Law 4:6; 10:4-7; 21:12; 23; Hes 3:28; Ebr 9:1-2; Law 26:11-12; Hes 5:3; Kum 12:11; 1Fal 6:13; Zek 2:10; 2Kor 7:16; Ufu 21:3

[h]**25:9** Kut 26:30; 27:8; 31:11; 39:42-43; 1Nya 28:11, 19; Mdo 7:44; Ebr 8:5; Hes 8:4

[i]**25:10** Kum 10:1-5; 1Fal 6:19; Ebr 9:4

[j]10 Dhiraa mbili na nusu ni sawa na sentimita 112.5.

[k]10 Dhiraa moja na nusu ni sawa na sentimita 67.5.

[l]**25:11** Kut 30:3-4

[m]**25:13** Kut 27:6; 30:5; 37:28

[n]**25:14** Kut 27:7; 40:20; 1Nya 15:15

[o]**25:15** 1Fal 8:8

[p]**25:16** Kut 16:34; 1Fal 8:8; Kum 31:26

[q]**25:17** Law 16:13; Rum 3:25

[r]**25:18** Kut 26:1, 35; 1Fal 6:23-27; 2Nya 3:10-13; Ebr 9:5

[s]**25:20** Mwa 3:24; Kut 37:9; 1Fal 8:7; 1Nya 28:18; Ebr 9:5

[t]**25:21** Kut 26:34; 40:20; Kum 10:5; Kut 16:34; Ebr 9:4

kifuniko juu ya hilo Sanduku. 22 [a]Hapo juu
ya hicho kifuniko, kati ya hao makerubi
wawili walioko juu ya hilo Sanduku la
Ushuhuda, hapo ndipo nitakapokutana
nawe na kukupa maagizo yangu kwa ajili
ya Waisraeli.

*Meza Ya Mikate Ya Wonyesho*

**(Kutoka 37:10-16)**

23 [b]"Tengeneza meza ya mbao za mshita
yenye urefu wa dhiraa mbili,[c] upana wa
dhiraa moja, na kimo cha dhiraa moja
na nusu. 24 Ifunike kwa dhahabu safi,
na kuitengenezea ukingo wa dhahabu
kuizunguka pande zote. 25 Kisha tengeneza
upapi wenye upana wa nyanda nne,[d] na
ufanyie ule upapi ukingo wa dhahabu
kuuzunguka pande zote. 26 Tengeneza pete
nne za dhahabu kwa ajili ya meza hiyo, na
uzifungie kwenye pembe nne, pale penye
miguu yake minne. 27 Pete hizo zitakuwa
karibu na ukingo ule ili kuishikilia ile
mipiko itakayotumika kuibebea hiyo
meza. 28 Tengeneza mipiko hiyo kwa mbao
za mshita, uifunike na dhahabu, uitumie
kubeba hiyo meza. 29 [e]Tengeneza sahani
zake na masinia yake kwa dhahabu safi,
pamoja na bilauri na bakuli zake kwa ajili
ya kumiminia sadaka. 30 [f]Utaweka mikate
ya Wonyesho juu ya meza hii iwe mbele
yangu daima.

*Kinara Cha Taa*

**(Kutoka 37:17-24)**

31 [g]"Tengeneza kinara cha taa cha dhahabu
safi iliyofuliwa vizuri katika kitako chake na
ufito wake; vikombe vyake vinavyofanana
na ua, matovu yake na maua yake viwe kitu
kimoja. 32 [h]Matawi sita yatatokeza kuanzia
ule ufito wa katikati wa kinara cha taa:
matawi matatu upande mmoja na matatu
upande mwingine. 33 Vikombe vitatu vya
mfano wa maua ya mlozi yenye matovu
na maua vitakuwa katika tawi moja,
vikombe vitatu katika tawi jingine, na vivyo
hivyo kwa matawi yote sita yanayotokeza
kwenye kile kinara cha taa. 34 Juu ya kinara
chenyewe vitakuwepo vikombe vinne
vya mfano wa maua ya mlozi yakiwa na
matovu yake na maua yake. 35 Tovu moja
litakuwa chini ya jozi ya kwanza ya matawi
yaliyotokeza kwenye kinara cha taa, tovu
la pili chini ya jozi ya pili, nalo tovu la
tatu chini ya jozi ya tatu, yaani matawi
sita kwa jumla. 36 [i]Matovu na matawi yote
yatakuwa kitu kimoja na kile kinara cha
taa, yakifuliwa kwa dhahabu safi.

37 [j]"Kisha tengeneza taa zake saba na
uziweke juu ya kinara hicho ili ziangaze
mbele yake. 38 [k]Mikasi ya kusawazishia
tambi, pamoja na masinia, zote zitakuwa
za dhahabu safi. 39 Utatumia talanta moja[l]
ya dhahabu safi kutengeneza hicho kinara
na vifaa vyake vyote. 40 [m]Hakikisha kuwa
umevitengeneza sawasawa na ule mfano
ulioonyeshwa kule mlimani.

---

[a]**25:22** Hes 7:89; 1Sam 4; 4; 2Sam 6:2; 22:11; 2Fal 19:15; 1Nya 13:6; 28:18; Za 18:10; Isa 37:16; Kut 19:3; 29:42; 30:6, 36; Law 16:2; Hes 17:4

[b]**25:23** Yer 3:16; Kut 26:35; 40:4, 22; Law 24:6; Hes 3:31; 1Fal 7:48; 1Nya 28:16; 2Nya 4:8, 19; Eze 41:22; 44:16; Ebr 9:2

[c]23 Dhiraa mbili ni sawa na sentimita 90.

[d]25 Nyanda nne ni sawa na sentimita 8.

[e]**25:29** Hes 4:7

[f]**25:30** Kut 35:13; 39:36; 40:4, 23; Law 24:5-9; Hes 4:7; 1Sam 21:4-6; 1Fal 7:48; 1Nya 23:29

[g]**25:31** Kut 26:35; 31:8; 35:14; 39:37; Law 24:4; Hes 3:31; 1Fal 7:49; 2Nya 4:7; Zek 4:2; Ebr 9:2; Ufu 1:12

[h]**25:32** Hes 8:4; Kut 37:18, 19

[i]**25:36** Hes 8:4

[j]**25:37** Kut 27:21; 30:8; Law 24:3-4; Hes 8:2; 1Sam 3:3; 2Nya 13:11; Ufu 1:12

[k]**25:38** Hes 4:9

[l]39 Talanta moja ya dhahabu ni sawa na kilo 34.

[m]**25:40** Hes 8:4; Mdo 7:44; Ebr 8:5; Kut 26:30; 1Nya 28:11, 19

*Maskani Ya Mungu*

**(Kutoka 36:8-38)**

26 [a]"Tengeneza maskani kwa mapazia
kumi ya kitani iliyosokotwa vizuri
na nyuzi za rangi ya buluu, za zambarau,
na za rangi nyekundu, naye fundi stadi
atatarizi makerubi kwenye mapazia hayo.
2 Mapazia yote yatatoshana kwa ukubwa:
kila moja litakuwa na urefu wa dhiraa
ishirini na nane,[b] na upana wa dhiraa nne[c]
3 [d]Unganisha mapazia matano pamoja;
fanya vivyo hivyo kwa hayo mengine
matano. 4 [e]Tengeneza vitanzi vya kitambaa
cha buluu kwenye upindo wa pazia la
mwisho la fungu la kwanza, na ufanye
vivyo hivyo na pazia la fungu la mwisho.
5 Fanya vitanzi hamsini katika pazia mmoja,
na vitanzi vingine hamsini kwenye pazia la
mwisho la fungu hilo lingine, nazo vitanzi
vyote vielekeane. 6 Kisha tengeneza vifungo
hamsini vya dhahabu ili vitumike kufunga
na kuunganisha mapazia pamoja kufanya
Hema liwe kitu kimoja.

7 [f]"Tengeneza mapazia kumi na moja
ya singa za mbuzi kwa ajili ya kufunika
maskani. 8 Mapazia hayo kumi na moja
yatakuwa na kipimo kimoja, yaani urefu
wa dhiraa thelathini,[g] na upana wa dhiraa
nne. 9 Unganisha hayo mapazia matano
yawe fungu moja, na hayo mengine sita
yawe fungu lingine. Kunja hilo pazia la sita
mara mbili mbele ya maskani. 10 Tengeneza
vitanzi hamsini kwenye upindo wa pazia
la mwisho la fungu moja, na vivyo hivyo
kwenye upindo wa pazia la mwisho la fungu
hilo lingine. 11 Kisha tengeneza vifungo
hamsini vya shaba, uviingize katika vile
vitanzi ili kukaza hema pamoja kuwa kitu
kimoja. 12 Kuhusu kile kipande cha ziada
cha pazia la Hema, nusu ya hilo pazia
lililobaki litaning'inizwa upande wa nyuma
wa Hema. 13 Mapazia ya hema yatakuwa
na urefu wa dhiraa moja zaidi pande zote,
sehemu itakayobaki itaning'inia pande
zote za Hema ili kuifunika. 14 [h]Tengeneza
kifuniko cha hema kwa ngozi za kondoo
dume zilizotiwa rangi nyekundu, na juu
yake kifuniko cha ngozi za pomboo.[i]

15 "Tengeneza mihimili ya kusimamisha
ya mti wa mshita kwa ajili ya maskani.
16 Kila mhimili uwe na urefu wa dhiraa
kumi[j] na upana wa dhiraa moja na nusu,
17 zikiwa na ndimi mbili zilizo sambamba
kila mmoja na mwingine. Tengeneza
mihimili yote ya maskani jinsi hii.
18 Tengeneza mihimili ishirini kwa ajili ya
upande wa kusini wa maskani, 19 [k]kisha
tengeneza vitako arobaini vya fedha vya
kuweka chini ya hiyo mihimili, vitako
viwili kwa kila mhimili, kimoja chini ya
kila ulimi. 20 Kuhusu upande wa kaskazini
wa maskani, tengeneza mihimili ishirini
21 na vitako arobaini vya fedha, viwili
chini ya kila mhimili. 22 Kisha tengeneza
mihimili sita kwa mwisho ulio mbali, yaani
upande wa magharibi wa maskani, 23 na
pia utengeneze mihimili miwili ya pembe
za upande ulio mbali. 24 Katika pembe hizi
mbili ni lazima mihimili yake iwe miwili
kuanzia chini mpaka juu, na iingizwe
kwenye pete moja; mihimili ya pembe
hizi mbili itafanana. 25 Kwa hiyo itakuwepo
mihimili minane, na vitako kumi na sita vya
fedha, viwili chini ya kila mhimili.

26 [l]"Pia tengeneza mataruma ya mti wa
mshita: matano kwa ajili ya mihimili ya
upande mmoja wa maskani, 27 matano kwa
ajili ya mihimili ya upande mwingine, na
matano kwa ajili ya mihimili ya upande
wa magharibi, mwisho kabisa mwa
maskani. 28 Taruma la katikati litapenya
katikati ya mihimili kutoka mwisho mmoja
hadi mwisho mwingine. 29 Funika hiyo
mihimili kwa dhahabu, kisha tengeneza

---

[a]**26:1** Kut 29:42; 40:2; Law 8:10; Hes 1:50; Yos 22:19-20; 2Sam 7:2; 1Fal 1:30; Mdo 7:44; Ebr 8:2-5; 13:10; Ufu 21:3; Kut 25:18

[b]2 Dhiraa 28 ni sawa na mita 13.

[c]2 Dhiraa nne ni sawa na mita 1.8.

[d]**26:3** 1Kor 12:4-12

[e]**26:4** Efe 4:13; Kol 2:2, 19

[f]**26:7** Kut 36:14

[g]8 Dhiraa 30 ni sawa na mita 13.5.

[h]**26:14** Kut 36:19; Hes 3:25; 4:25

[i]14 *Pomboo* hapa ina maana ya mnyama mwenye ngozi laini aishiye kwenye milima yenye misitu, au pengine nguva au sili.

[j]16 Dhiraa 10 ni sawa na mita 4.5.

[k]**26:19** Kut 38:27

[l]**26:26** Kut 36:31; Rum 15:1; Gal 6:2

pete za dhahabu ambazo zitashikilia hayo mataruma. Pia funika hayo mataruma kwa dhahabu.

30 [a]“Simamisha Hema sawasawa na mfano ulioonyeshwa kule mlimani.

31 [b]“Tengeneza pazia la nyuzi za rangi ya buluu, za zambarau, na za rangi nyekundu na kitani safi iliyosokotwa vizuri, naye fundi stadi atirizi makerubi kwenye hilo
pazia. 32 Litundike kwa kulabu za dhahabu kwenye nguzo nne za mti wa mshita ambazo zimefunikwa kwa dhahabu, zikiwa zimesimamishwa kwenye vitako vinne vya fedha.
33 [c]Ning’iniza pazia hilo kwenye vifungo, kisha weka Sanduku la Ushuhuda nyuma ya pazia. Pazia litatenganisha Mahali Patakatifu kutoka Patakatifu pa Patakatifu.
34 [d]Weka kifuniko cha kiti cha rehema juu ya Sanduku la Ushuhuda ndani ya Patakatifu
pa Patakatifu. 35 [e]Weka meza nje ya pazia upande wa kaskazini wa Hema, kisha weka kinara cha taa upande wa kusini wa Hema.

36 [f]“Kwa ajili ya ingilio la hema, tengeneza pazia la nyuzi za rangi ya buluu, za zambarau, na za rangi nyekundu na kitani safi iliyosokotwa vizuri, kazi ya mtarizi.
37 [g]Tengeneza kulabu za dhahabu kwa ajili ya hilo pazia, na nguzo tano za mshita zilizofunikwa kwa dhahabu. Kisha mimina vitako vitano vya shaba kwa ajili yake.

*Madhabahu Ya Sadaka Ya Kuteketezwa*

**(Kutoka 38:1-7)**

27 [h]“Jenga madhabahu ya mbao za mti wa mshita, kimo chake kiwe dhiraa tatu;[i] itakuwa mraba, urefu wake dhiraa tano,[j]
na upana wake dhiraa tano. 2 [k]Tengeneza upembe kwenye kila pembe ya hizo pembe nne, ili zile pembe na madhabahu ziwe zimeungana, na ufunike madhabahu
kwa shaba. 3 [l]Tengeneza vyombo vyake vyote kwa shaba: vyungu vyake vya kuondolea majivu, masepetu, mabakuli ya kunyunyizia, uma za nyama, na vyombo vya
kuchukulia moto. 4 Kisha tengenezea hayo madhabahu wavu wa shaba, na utengeneze pete za shaba kwenye kila moja ya hizo
pembe nne za huo wavu. 5 Weka wavu huo chini ya ukingo wa madhabahu ili ufikie
nusu ya kimo cha madhabahu. 6 [m]Tengeneza mipiko ya mti wa mshita kwa ajili ya
madhabahu, na uifunike kwa shaba. 7 [n]Hiyo mipiko itaingizwa kwenye zile pete ili iwe pande mbili za madhabahu inapobebwa.
8 [o]Tengeneza madhabahu yawe na uvungu ndani yake ukitumia mbao. Utaitengeneza sawasawa na vile ulivyoonyeshwa mlimani.

*Ua Wa Kukutania*

**(Kutoka 38:9-20)**

9 [p]“Tengeneza ua kwa ajili ya Hema la Kukutania. Upande wa kusini utakuwa na urefu wa dhiraa mia moja,[q] na utakuwa na mapazia ya kitani iliyosokotwa vizuri,
10 pamoja na nguzo ishirini na vitako vya shaba ishirini, na kulabu na tepe za fedha
juu ya hizo nguzo. 11 Upande wa kaskazini

---

[a]**26:30** Kut 40:2; 25:9; Hes 9:15; Ebr 8:5; Mdo 7:44; Ebr 8:5
[b]**26:31** Hes 4:5; 2Nya 3:14; Mt 27:51; Lk 23:45; Ebr 9:3; Kut 25:18; 36:35; Law 16:2; Kut 25:18; 36:35
[c]**26:33** Kut 27:21; 35:12; 40:2-3, 21; Law 16:2; Hes 3:31; 4:5; 2Nya 3:14; Law 16:2, 16; 1Fal 6:16; 7:50; 8:6; 2Nya 3:8; 5:7; Eze 41:5; Ebr 9:2-3
[d]**26:34** Kut 25:21; 30:6; 37:6; Law 16:2; Ebr 9:5
[e]**26:35** Kut 25:23; Ebr 9:2; Kut 25:31
[f]**26:36** Kut 35:15; 40:5; 28; Za 45:14; Eze 16:10; 26:16; 27:7
[g]**26:37** Kut 38:1
[h]**27:1** Kut 20:24; 40:6; 1Fal 8:64
[i]1 Dhiraa 3 ni sawa na mita 1.35.
[j]1 Dhiraa 5 ni sawa na mita 2.25.
[k]**27:2** Kut 29:12; 30:2; 37:25; Law 4:7; 1Fal 1:50; 2:28; Za 118:27; Yer 17:1; Eze 43:15; Amo 3:14; Zek 9:15
[l]**27:3** Hes 7:13; 1Fal 7:40-45; 2Fal 12:13; Hes 4:14; 1Nya 28:17; Yer 52:18
[m]**27:6** Kut 25:13-14, 28
[n]**27:7** Hes 4:15; Isa 52:11
[o]**27:8** Kut 25:9, 40; Ebr 8:5; Mdo 7:44
[p]**27:9** Kut 35:17; 40:8, 33; Law 6:16, 26; Eze 40:14; 42:1
[q]9 Dhiraa 100 ni sawa na mita 45.

utakuwa na urefu wa dhiraa mia moja, nao utakuwa na mapazia, pamoja na nguzo ishirini na vitako vya shaba ishirini, pamoja na kulabu na tepe za fedha juu ya hizo nguzo.

12 “Upande wa magharibi wa ua utakuwa na upana wa dhiraa hamsini,[a] nao utakuwa na mapazia, na nguzo kumi na vitako vyake kumi. 13 Upande wa mwisho wa mashariki jua linakochomoza, ua pia utakuwa na upana wa dhiraa hamsini. 14 Mapazia yenye urefu wa dhiraa kumi na tano yatakuwa upande mmoja wa ingilio, pamoja na nguzo tatu na vitako vitatu. 15 Kutakuwepo tena na mapazia ya dhiraa kumi na tano[b] kwa upande mwingine wa ingilio, pamoja na nguzo tatu na vitako vitatu.

16 [c]“Kuhusu ingilio la ua, weka pazia lenye urefu wa dhiraa ishirini[d] la nyuzi za rangi ya buluu, za zambarau, na za rangi nyekundu pamoja na kitani iliyosokotwa vizuri, kazi ya mtarizi. Pazia hilo litashikiliwa na nguzo nne na vitako vinne. 17 Nguzo zote zinazozunguka ua zitakuwa na tepe na kulabu za fedha, na vitako vya shaba. 18 Ua wa kukutania utakuwa na urefu wa dhiraa mia moja na upana wa dhiraa hamsini, ukiwa na mapazia ya kitani yaliyosokotwa vizuri yenye urefu wa dhiraa tano kwenda juu na vitako vya shaba. 19 Vyombo vingine vyote vinavyotumika katika maskani kwa shughuli yoyote, pamoja na vigingi vyote na hata vile vya ua, vitakuwa vya shaba.

*Mafuta Ya Kinara Cha Taa*

**(Walawi 24:1-4)**

20 [e]“Utawaamuru Waisraeli wakuletee mafuta safi ya zeituni yaliyokamuliwa kwa ajili ya mwanga ili zile taa ziwake mfululizo. 21 [f]Katika Hema la Kukutania, nje ya pazia lililo mbele ya Sanduku la Ushuhuda, Aroni na wanawe watahakikisha kuwa taa hizo zinawaka kuanzia jioni mpaka asubuhi mbele za BWANA. Hili litakuwa agizo la milele miongoni mwa Waisraeli kwa vizazi vyote vijavyo.

*Mavazi Ya Kikuhani*

**(Kutoka 39:1-7)**

28 [g]“Mtwae Aroni ndugu yako aliyeletwa kwako kutoka miongoni mwa Waisraeli, pamoja na wanawe Nadabu, Abihu, Eleazari na Ithamari, ili wanitumikie katika kazi ya ukuhani. 2 [h]Mshonee Aroni ndugu yako mavazi matakatifu ili yampe ukuu na heshima. 3 [i]Waambie mafundi stadi wote niliowapa hekima katika shughuli hiyo wamtengenezee Aroni mavazi hayo, ili awekwe wakfu, anitumikie katika kazi ya ukuhani. 4 [j]Haya ndiyo mavazi watakayoshona: kifuko cha kifuani, kisibau, kanzu, joho lililorembwa, kilemba na mshipi. Mavazi haya yatashonwa kwa ajili ya ndugu yako Aroni na wanawe ili wanitumikie katika kazi ya ukuhani. 5 [k]Waambie watumie dhahabu na nyuzi za rangi ya buluu, za zambarau, na za rangi nyekundu pamoja na kitani safi.

*Kisibau*

6 [l]“Tengeneza kisibau cha dhahabu, na nyuzi za rangi ya buluu, za zambarau, za rangi nyekundu na kitani safi iliyosokotwa, kazi ya fundi stadi. 7 Kitakuwa na vipande viwili vya mabegani vilivyoshikizwa kwenye pembe zake mbili ili kufungia kisibau. 8 [m]Mshipi wa kiunoni uliofumwa kwa ustadi utafanana nacho: utakuwa kitu kimoja na hicho kisibau, nao utengenezwe kwa dhahabu na nyuzi za rangi ya buluu,

---

[a]12 Dhiraa 50 ni sawa na mita 22.5.
[b]15 Dhiraa 15 ni sawa na mita 6.75.
[c]**27:16** Kut 40:33; 36:37
[d]16 Dhiraa 20 ni sawa na mita 9.
[e]**27:20** Kut 25:6; Law 24:2
[f]**27:21** Kut 28:43; 29:42; 30:36; 33:7; Law 6:26; 8:3, 31; Hes 31:54; Yos 18:1; 1Fal 1:38-39; Kut 16:34; 25:37; 29:9; 30:21; Law 3:17; 16:34; 17:7; Hes 18:23; 19:21; 1Sam 30:25
[g]**28:1** Law 8:30; Za 99:9; Ebr 5; 4; Kut 6:23; 24:9; Law 8:2; 21:1; Hes 18:1-7; Kum 18:5; 1Sam 2:28; Ebr 5:1
[h]**28:2** Kut 29:5; 31:10; 35:19; Law 8:7-9; 16:32; Hes 20:26-28
[i]**28:3** Kut 31:6; 35:10, 25, 35; 36:1; 31:3; Kum 34:9; Isa 11:2
[j]**28:4** Kut 25:7; Law 10:5
[k]**28:5** Kut 25:4-7; 25:4-7
[l]**28:6** Kut 39:2; Law 8:7
[m]**28:8** Kut 29:5

za zambarau, na nyekundu na kwa kitani
iliyosokotwa vizuri.
9 [a]"Chukua vito viwili vya shohamu, na
uchore juu yake majina ya wana wa Israeli
10 kufuatana na walivyozaliwa: majina sita
katika kito kimoja, na mengine sita katika
kito kingine. 11 Yachore majina ya wana wa
Israeli juu ya vito hivyo viwili kama vile
sonara anavyochonga muhuri. Kisha uvitie
vito hivyo katika vijalizo vya dhahabu,
12 [b]na uvifungie juu ya vipande vya mabega
ya kisibau yawe kama vito vya ukumbusho
kwa wana wa Israeli. Aroni atavaa majina
hayo mabegani mwake kama kumbukumbu
mbele za BWANA. 13 Tengeneza vijalizo vya
dhahabu 14 na mikufu miwili ya dhahabu
safi iliyosokotwa kama kamba, na uifunge
mikufu hiyo kwenye vijalizo.

*Kifuko Cha Kifuani*

**(Kutoka 39:8-21)**

15 [c]"Fanyiza kifuko cha kifuani kwa
ajili ya kufanya maamuzi, kazi ya fundi
stadi. Kitengeneze kama kile kisibau: cha
dhahabu, na nyuzi za rangi ya buluu, za
zambarau, na za rangi nyekundu, cha
kitani safi iliyosokotwa. 16 Kitakuwa cha
mraba, chenye urefu wa shibiri moja[d] na
upana wa shibiri moja, na kikunjwe mara
mbili. 17 [e]Kisha weka safu nne za vito vya
thamani juu yake. Safu ya kwanza itakuwa
na akiki, yakuti manjano na zabarajadi;
18 katika safu ya pili itakuwa na almasi,
yakuti samawi na zumaridi; 19 safu ya tatu
itakuwa na hiakintho, akiki nyekundu na
amethisto; 20 [f]na safu ya nne itakuwa na
krisolitho, shohamu na yaspi. Yote yatiwe
kwenye vijalizo vya dhahabu. 21 [g]Patakuwa
na vito kumi na viwili, kila kimoja kwa jina
mojawapo la wana wa Israeli, kila kimoja
kichorwe kama muhuri kikiwa na jina
mojawapo la yale makabila kumi na mawili.
22 "Kwa ajili ya kile kifuko cha kifuani,
tengeneza mikufu ya dhahabu safi,
iliyosokotwa kama kamba. 23 Tengeneza pete
mbili za dhahabu kwa ajili yake, uzifungie
kwenye pembe mbili za hicho kifuko cha
kifuani. 24 Funga ile mikufu miwili ya
dhahabu kwenye hizo pete zilizo katika
pembe za hicho kifuko cha kifuani, 25 nazo
zile ncha nyingine za mkufu zifunge kwenye
vile vijalizo viwili, na uzishikamanishe na
vile vipande vya mabega vya kile kisibau
upande wa mbele. 26 Tengeneza pete mbili
za dhahabu, uzishikamanishe kwenye
pembe mbili za chini, upande wa ndani
wa kifuko cha kifuani karibu na kisibau.
27 Tengeneza pete nyingine mbili za
dhahabu, na uzishikamanishe sehemu ya
chini ya vipande vya mabega upande wa
mbele wa kile kisibau, karibu na pindo juu
kidogo ya mshipi wa kiunoni wa kisibau.
28 Pete za kifuko cha kifuani zitafungwa
kwenye pete zile za kisibau kwa kamba
ya buluu, ziunganishwe na ule mshipi wa
kiunoni, ili kifuko cha kifuani kisisogee
kutoka kwenye kile kisibau.
29 [h]"Wakati wowote Aroni aingiapo
Mahali Patakatifu, atakuwa na yale majina
ya wana wa Israeli moyoni mwake juu ya
kile kifuko cha kifuani cha uamuzi kama
kumbukumbu ya kudumu mbele za BWANA.
30 [i]Pia weka Urimu na Thumimu[j] ndani ya
kifuko cha kifuani, yawe juu ya moyo wa
Aroni kila mara aingiapo mbele za BWANA.
Kwa hiyo siku zote Aroni atakuwa na uwezo

---

[a]**28:9** Wim 8:6; Isa 44:16; Hag 2:23
[b]**28:12** Kum 33:12; Ay 31:36; Kut 30:16; Hes 10:10; 31:54; Yos 4:7; Zek 6:14; Kut 39:7; Mwa 9:12-17; Kut 12:14; Mk 14:9; Mdo 10:4; 1Kor 11:24, 25
[c]**28:15** Kut 25:7; 39:8; Law 8:8; Isa 59:17; 1The 5:7; Efe 6:14
[d]16 Shibiri moja ni sawa na sentimita 22.
[e]**28:17** Eze 28:13; Ufu 21:19-20; Kut 30:10; Mal 3:17
[f]**28:20** Eze 1:16; 10:9; Dan 10:6
[g]**28:21** Yos 4:8; Ufu 21:12; Hes 1:5; 2:3; Ufu 7:4-8; 21:12
[h]**28:29** Wim 8:6; Isa 49:15, 16; Ebr 9:24
[i]**28:30** Law 8:8; Hes 27:21; Kum 33:8; 1Sam 28:6; Ezr 2:63; Neh 7:65
[j]30 Urimu na Thumimu maana yake ni Nuru na Kweli; vifaa hivi viliwekwa kwenye kifuko cha juu cha kisibau cha kuhani mkuu ili kujua mapenzi ya Mungu kwenye mambo ya kutatanisha.

kufanya maamuzi kwa ajili ya wana wa
Israeli mbele za Bwana.

*Mavazi Mengine Ya Kikuhani*

**(Kutoka 39:22-31)**

31 [a]“Shona joho la kisibau lote kwa
kitambaa cha rangi ya buluu tupu, 32 na
katikati uweke nafasi ya kuingizia kichwa.
Kutakuwa na utepe uliofumwa, unaofanana
na ukosi kuizunguka nafasi hiyo, ili
isichanike. 33 [b]Tengeneza makomamanga
ya nyuzi za rangi ya buluu, za zambarau, na
za rangi nyekundu kuzunguka pindo la hilo
joho, na uweke pia vikengele vya dhahabu
kati ya hayo makomamanga. 34 Hivyo
vikengele vya dhahabu na makomamanga
vitapishana kuzunguka upindo wa joho
lile. 35 Ni lazima Aroni alivae anapofanya
huduma. Sauti ya hivyo vikengele itasikika
anapoingia na kutoka Mahali Patakatifu
mbele za Bwana, ili asije akafa.
36 [c]“Tengeneza bamba la dhahabu safi
na uchore juu yake maneno haya kama
vile muhuri huchorwa: Mtakatifu kwa
Bwana. 37 Lifunge hilo bamba kwa kamba
ya buluu kwenye kilemba, nalo ni lazima
liwe mbele ya kilemba. 38 [d]Aroni alivae
bamba hilo kwenye paji la uso wake, naye
atachukua hatia kuhusu sadaka takatifu za
Waisraeli wanazoweka wakfu, sadaka za
aina yoyote. Litakuwa kwenye paji la uso
wa Aroni daima ili zikubalike kwa Bwana.
39 [e]“Fuma koti la kitani safi na ufanye
kilemba cha kitani safi. Mshipi uwe ni kazi
ya mtarizi. 40 [f]Watengenezee wana wa Aroni
makoti, mishipi na kofia, ili kuwapa ukuu na
heshima. 41 [g]Baada ya kumvika Aroni ndugu
yako pamoja na wanawe nguo hizi, watie
mafuta na kuwabariki. Waweke wakfu ili
wanitumikie katika kazi ya ukuhani.
42 [h]“Watengenezee nguo za ndani za kitani
zitakazofunika mwili, kutoka kiunoni hadi
mapajani. 43 [i]Aroni na wanawe ni lazima
wavae haya kila wanapoingia katika Hema
la Kukutania au wanaposogelea madhabahu
wakati wa kutoa huduma katika Mahali
Patakatifu, ili wasije wakafanya kosa
wakafa.

“Haya yawe maagizo ya kudumu kwa
Aroni na vizazi vyake.

*Kuweka Wakfu Makuhani*

**(Walawi 8:1-36)**

29 [j]“Hili ndilo utakalofanya ili kuwaweka
wakfu makuhani ili wanitumikie mimi
katika kazi ya ukuhani: Chukua fahali
mchanga mmoja na kondoo dume wawili
wasio na dosari. 2 [k]Kutokana na unga laini
wa ngano usiotiwa chachu, tengeneza
mikate na maandazi yaliyokandwa
kwa mafuta, pamoja na mikate midogo
myembamba. 3 Viwekwe vyote ndani ya
kikapu na kuvitoa pamoja na yule fahali na
wale kondoo dume wawili. 4 [l]Kisha mlete
Aroni na wanawe kwenye lango la Hema la
Kukutania na uwaoshe kwa maji. 5 [m]Chukua
yale mavazi na umvike Aroni koti, joho la
kisibau na kisibau chenyewe pamoja na kile
kifuko cha kifuani. Mfungie hicho kisibau
kwa ule mshipi wa kiunoni uliosukwa kwa
ustadi. 6 [n]Weka kilemba kichwani mwake na
kuweka taji takatifu ishikamane na hicho

---

[a]**28:31** Kut 39:22; Law 8:7; 2Sam 6:14; Hos 3:4

[b]**28:33** Hes 13:23; 1Sam 14:2; 1Fal 7:18; Wim 4:3; Yer 52:22; Yoe 1:12; Hag 2:19

[c]**28:36** Kut 29:6; Law 8:9; Zek 14:20; Kut 39:30; 1Nya 16:29; Za 29:2; 93:5; Ebr 4:15; 7:26

[d]**28:38** Law 5:1; 10:17; 16:22; 22:9, 16; Hes 18:1; Isa 53:5-11; Eze 4:4-6; Ebr 9:28; 1Pet 2:24; Mwa 32:20; Law 22:20, 27; 23:11; Isa 56:7

[e]**28:39** Kut 29:6; Law 16:4; Eze 24:17-23; 44:18

[f]**28:40** Kut 29:8-9; 39:41; 40:14; Law 8:13; Eze 44:17

[g]**28:41** Kut 40:13; 29:7; Law 6:20; 10:7; 21:12; Hes 35:25; Kut 29:7-9; 30:30; 40:15; Law 4:3; 6:22; 8:1-36; Hes 3:3; Ebr 7:28

[h]**28:42** Law 6:10; 16:4, 23; Eze 44:18

[i]**28:43** Kut 27:21; 30:20-21; Law 16:13; 22:9; Hes 1:51; 4:15-20; 18:22

[j]**29:1** Law 20:7; Yos 3:5; 1Nya 15:12; Eze 43:23

[k]**29:2** Law 2:1-4; 6:19-23; Hes 6:15

[l]**29:4** Kut 40:12; Law 14:8; 16:4; Ebr 10:22

[m]**29:5** Kut 28:2; 28:8; Law 8:7

[n]**29:6** Kut 28:39; Isa 3:23; Zek 3:5; Kut 28:36

kilemba. 7 [a]Chukua yale mafuta ya upako
umimine juu ya kichwa chake. 8 [b]Walete
wanawe na uwavike makoti, 9 [c]pia uwavike
zile tepe za kichwani. Ndipo uwafunge
Aroni na wanawe mishipi. Ukuhani ni
wao kwa agizo la kudumu. Kwa njia hii
utamweka wakfu Aroni na wanawe.
10 [d]"Mlete yule fahali mbele ya Hema
la Kukutania, naye Aroni na wanawe
wataweka mikono yao juu ya kichwa chake.
11 [e]Mchinje huyo fahali mbele za BWANA
kwenye mlango wa Hema la Kukutania.
12 [f]Chukua sehemu ya damu ya huyo
fahali na kuipaka kwenye pembe za hayo
madhabahu kwa kidole chako, na damu
iliyobaki uimwage sehemu ya chini ya
madhabahu. 13 [g]Kisha chukua mafuta yote
ya huyo mnyama ya sehemu za ndani,
yale yanayofunika ini, figo zote mbili
pamoja na mafuta yake, uviteketeze juu
ya madhabahu. 14 [h]Lakini nyama ya huyo
fahali na ngozi yake na matumbo yake
utavichoma nje ya kambi. Hii ni sadaka
ya dhambi.
15 [i]"Chukua mmoja wa wale kondoo
dume, naye Aroni na wanawe wataweka
mikono yao juu ya kichwa chake. 16 Mchinje
huyo kondoo dume, chukua damu yake na
uinyunyize pande zote za hayo madhabahu.
17 Mkate huyo kondoo dume vipande
vipande na usafishe sehemu za ndani
pamoja na miguu, ukiviweka pamoja
na kichwa na vipande vingine. 18 [j]Kisha
mteketeze huyo kondoo dume mzima juu ya
madhabahu. Hii ni sadaka ya kuteketezwa
kwa BWANA, harufu ya kupendeza, sadaka
iliyotolewa kwa BWANA kwa moto.
19 [k]"Mchukue yule kondoo dume
mwingine, naye Aroni na wanawe
waweke mikono yao juu ya kichwa chake.
20 [l]Mchinje, uchukue sehemu ya damu yake
na kuipaka kwenye masikio ya Aroni na
wanawe, kwenye vidole gumba vya mikono
yao ya kuume, pia kwenye vidole gumba
vya miguu yao ya kuume. Kisha nyunyiza
hiyo damu pande zote za madhabahu.
21 [m]Pia chukua sehemu ya damu iliyo juu
ya madhabahu na sehemu ya mafuta ya
upako, umnyunyizie Aroni na mavazi yake,
pia wanawe na mavazi yao. Ndipo Aroni na
wanawe pamoja na mavazi yao watakuwa
wamewekwa wakfu.
22 "Chukua mafuta ya huyu kondoo
dume, mafuta ya mkia, mafuta ya sehemu
za ndani yale yanayofunika ini, figo zote
mbili na mafuta yake, pamoja na paja la
kulia. (Huyo ndiye kondoo dume kwa ajili
ya kuwaweka wakfu.) 23 [n]Kutoka kwenye
kile kikapu chenye mikate iliyotengenezwa
bila chachu, kilichoko mbele za BWANA,
chukua mkate, andazi lililokandwa kwa
mafuta na mkate mdogo mwembamba.
24 [o]Viweke vitu hivi vyote mikononi mwa
Aroni na wanawe na uviinue mbele za
BWANA kuwa sadaka ya kuinuliwa. 25 [p]Kisha
vichukue vitu hivyo kutoka mikononi
mwao, uviteketeze juu ya madhabahu
pamoja na sadaka ya kuteketezwa kuwa
harufu nzuri ya kupendeza kwa BWANA,
sadaka iliyotolewa kwa BWANA kwa moto.
26 [q]Baada ya kuchukua kidari cha huyo
kondoo dume wa kuwekwa wakfu kwa
Aroni, kiinue mbele za BWANA kuwa sadaka
ya kuinuliwa, nayo itakuwa fungu lako.

---

[a]**29:7** Kut 28:41; 30:25-31; 37:29; Law 21:10; 1Sam 10:1; Za 89:20; 133:2; 141:5; Hes 35:25; Za 133:1, 2; Isa 61:1
[b]**29:8** Kut 28:4; Law 16:4
[c]**29:9** Kut 28:40; 27:21; 40:15; Hes 3:10; 18:7; 25:13; Kum 18:5; Amu 17:5; 1Sam 2:30; 1Fal 12:31
[d]**29:10** Law 1:4; 4:15; 16:21; Hes 8:12
[e]**29:11** Law 1:5, 11; 4:24; 6:16, 25; 14:13
[f]**29:12** Kut 27:2; Law 4:7; 9:9
[g]**29:13** Law 1:8; 3:3-9; 4:10; 6:12; 9:10; Hes 18:17; 1Sam 2:15; 1Fal 8:64; 2Nya 7:7; 29:35; 35:14; Isa 43:24; Eze 44:15; Kut 12:9
[h]**29:14** Nah 3:6; Mal 2:3; Law 4:12, 21; 16:17; Hes 19:3-5; Ebr 13:11; Hes 4:12, 21
[i]**29:15** 2Nya 29:23; 29:18; Mwa 8:21; 2Kor 2:15
[j]**29:18** Mwa 8:21; 2Kor 2:15
[k]**29:19** Kut 30:25; Law 8:30
[l]**29:20** Law 14:14, 25; 1:5; 3:2
[m]**29:21** Ebr 9:22; Kut 30:25-31
[n]**29:23** Law 8:26
[o]**29:24** Law 7:30; 9:21; 10:15; 14:12; 23:11, 20; Hes 6:20; 8:11-15
[p]**29:25** Law 8:28
[q]**29:26** Law 7:31-34

27 [a]“Weka wakfu zile sehemu za kondoo
dume aliyetumika kwa kumweka wakfu
Aroni na wanawe: kidari kile kilichoinuliwa
na lile paja lililotolewa. 28 [b]Siku zote hili
litakuwa fungu la kawaida kutoka kwa
Waisraeli kwa ajili ya Aroni na wanawe.
Hili ni toleo la Waisraeli watakalotoa kwa
BWANA kutoka sadaka zao za amani.
29 [c]“Mavazi matakatifu ya Aroni yatakuwa
ya wazao wake ili kwamba waweze kutiwa
mafuta na kuwekwa wakfu wakiwa
wameyavaa. 30 [d]Mwana atakayeingia mahali
pake kuwa kuhani na kuja kwenye Hema
la Kukutania kuhudumu katika Mahali
Patakatifu atayavaa kwa siku saba.
31 [e]“Chukua nyama ya huyo kondoo dume
wa kuwaweka wakfu uipike katika Mahali
Patakatifu. 32 [f]Aroni na wanawe wataila
ile nyama ya huyo kondoo dume pamoja
na ile mikate iliyo kwenye hicho kikapu
wakiwa hapo ingilio la Hema la Kukutania.
33 [g]Watakula sadaka hizi ambazo upatanisho
ulifanywa kwazo kwa ajili ya kuwaweka
wakfu na kuwatakasa. Lakini hakuna mtu
mwingine yeyote anayeruhusiwa kuvila,
kwa sababu ni vitakatifu. 34 [h]Ikiwa nyama
yoyote ya huyo kondoo dume iliyotumika
kwa kuwaweka wakfu au mkate wowote
umebaki mpaka asubuhi, vichomwe.
Kamwe visiliwe, kwa sababu ni vitakatifu.
35 [i]“Hivyo utamfanyia Aroni na wanawe
kila kitu kama vile nilivyokuamuru:
Utachukua muda wa siku saba kuwaweka
wakfu. 36 [j]Utatoa dhabihu ya fahali kila
siku kuwa sadaka ya dhambi ili kufanya
upatanisho. Takasa madhabahu kwa
kufanya upatanisho kwa ajili yake, nayo
uitie mafuta na kuiweka wakfu. 37 [k]Kwa
muda wa siku saba fanya upatanisho kwa
ajili ya madhabahu na kuiweka wakfu.
Ndipo madhabahu itakuwa takatifu sana
na chochote kitakachoigusa kitakuwa
kitakatifu.
38 [l]“Kwa kawaida hiki ndicho utakachotoa
juu ya madhabahu kila siku: wana-kondoo
wawili wenye umri wa mwaka mmoja.
39 [m]Utamtoa mmoja asubuhi na huyo
mwingine jioni. 40 [n]Pamoja na mwana-
kondoo wa kwanza utatoa efa moja[o] ya
unga wa ngano laini uliochanganywa na
robo ya hini[p] ya mafuta yaliyokamuliwa,
pamoja na robo ya hini ya divai kuwa
sadaka ya kinywaji. 41 [q]Huyo mwana-
kondoo mwingine mtoe dhabihu wakati
wa machweo pamoja na sadaka za unga
na za kinywaji kama vile ulivyofanya
asubuhi, kuwa harufu ya kupendeza, sadaka
iliyotolewa kwa BWANA kwa moto.
42 [r]“Kwa vizazi vijavyo itakuwa kawaida
kutoa sadaka hii ya kuteketezwa kila mara
kwenye ingilio la Hema la Kukutania mbele
za BWANA. Hapo ndipo nitakapokutana
na ninyi na kusema nanyi, 43 [s]Huko ndipo
nitakapokutana na Waisraeli, nalo Hema la
Kukutania litatakaswa na utukufu wangu.
44 [t]“Kwa hiyo nitaliweka wakfu Hema la
Kukutania pamoja na madhabahu, nami
nitamweka wakfu Aroni na wanawe ili
wanitumikie mimi katika kazi ya ukuhani.

---

[a]**29:27** Kut 22:29; Law 7:31-34; Hes 18:11-12; Kum 18:3
[b]**29:28** Law 7:30-34; 10:15
[c]**29:29** Kut 28:2; Law 16:4; Hes 20:28
[d]**29:30** Law 6:22; Hes 3:3; 20:28
[e]**29:31** Law 7:37; 2Nya 13:9; Law 10:14; Hes 19:9; Eze 42:13
[f]**29:32** Mt 12:4
[g]**29:33** Law 22:10-13
[h]**29:34** Kut 12; 10
[i]**29:35** Law 8:33
[j]**29:36** Ebr 10:11; Kut 30:10; Law 1:4; 4:20; 16:16; Hes 6:11; 8:12-19; 16:46; 23:25; 2Nya 29:24; Hes 7:10; Kut 40:10
[k]**29:37** Kut 30:28-29; 40:10; Eze 43:25; Mt 23:19
[l]**29:38** Law 23:2; Hes 28:3-8; 1Nya 16:40; 2Nya 8:13; Eze 46:13-15; Dan 12:11
[m]**29:39** Hes 28:4; 1Fal 18:36; 2Nya 13:11; Ezr 3:3; Za 141:2; Dan 9:21
[n]**29:40** Kut 30:24; Hes 15:4; 28:5; Mwa 35:14; Law 23:37; 2Fal 16:13
[o]40 Efa moja ni sawa na kilo 22.
[p]40 Robo ya hini ni sawa na lita moja.
[q]**29:41** 1Fal 18:29, 36; 2Fal 3:20; 16:15; Ezr 9:4-5; Za 141:2; Dan 9:21; Law 2:1; 5:3; 10:12; Hes 4:16; 6:17; 1Fal 8:64; Isa 43:23
[r]**29:42** Kut 30:8, 10, 21, 31; 31:13; Eze 46:15; Kut 26:1; 27:21; 25:22; 33:9, 11; Hes 7:89
[s]**29:43** Kut 33:18; 40:34; Law 9:6; 1Fal 8:11; 2Nya 5:14; 7:2; Za 26:8; 85:9; Eze 1:28; 43:5; Hag 1:8; 2:7
[t]**29:44** Law 21:15

45 [a]Ndipo nitakapofanya makao miongoni
mwa Waisraeli na kuwa Mungu wao. 46 [b]Nao
watajua kuwa Mimi Ndimi BWANA Mungu
wao, aliyewatoa Misri ili nipate kufanya
makao miongoni mwao. Mimi Ndimi
BWANA Mungu wao.

*Madhabahu Ya Kufukizia Uvumba*

**(Kutoka 37:25-28)**

30 [c]"Tengeneza madhabahu kwa mbao
za mshita kwa ajili ya kufukizia
uvumba. 2 [d]Madhabahu hayo yawe mraba,
urefu na upana wake dhiraa moja,[e] na
kimo cha dhiraa mbili,[f] nazo pembe zake
zitakuwa kitu kimoja nayo. 3 [g]Funika
hayo madhabahu juu na pande zote na
pia pembe zake kwa dhahabu safi, na
uifanyizie ukingo wa dhahabu kuizunguka.
4 [h]Tengeneza pete mbili za dhahabu kwa
ajili ya madhabahu chini ya huo ukingo,
ziwe mbili kila upande, za kushikilia hiyo
mipiko itumikayo kuibebea madhabahu.
5 [i]Tengeneza mipiko kwa miti ya mshita
na uifunike kwa dhahabu. 6 [j]Weka hayo
madhabahu mbele ya lile pazia lililo mbele
ya Sanduku la Ushuhuda, lililo mbele ya
kiti cha rehema kilicho juu ya Sanduku
la Ushuhuda, mahali ambapo nitakutana
nawe.

7 [k]"Itampasa Aroni kufukiza uvumba
wenye harufu nzuri juu ya madhabahu
kila siku asubuhi wakati anapowasha zile
taa. 8 [l]Itampasa afukize uvumba tena wakati
anapowasha taa wakati wa machweo ili
uvumba ufukizwe daima mbele za BWANA
kwa vizazi vijavyo. 9 [m]Usifukize uvumba
mwingine wowote juu ya madhabahu haya
au sadaka nyingine yoyote ya kuteketezwa
wala sadaka ya nafaka, wala usimimine
sadaka ya kinywaji juu yake. 10 [n]Mara moja
kwa mwaka Aroni atafanya upatanisho juu
ya pembe za hayo madhabahu. Upatanisho
huu wa mwaka lazima ufanywe kwa
damu ya sadaka ya upatanisho kwa ajili
ya dhambi kwa vizazi vijavyo. Ni takatifu
sana kwa BWANA."

*Fedha Ya Upatanisho*

11 Naye BWANA akamwambia Mose,
12 [o]"Utakapowahesabu Waisraeli, kila
mmoja lazima alipe kwa BWANA fidia kwa
ajili ya nafsi yake wakati wa kuhesabiwa
kwake. Ndipo hakutakuwa na pigo juu
yao unapowahesabu. 13 [p]Kila mmoja
anayekwenda upande wa wale waliokwisha
hesabiwa atatoa nusu shekeli,[q] kulingana
na shekeli ya mahali patakatifu, ambayo
ina uzito wa gera ishirini.[r] Hii nusu shekeli
ni sadaka kwa BWANA. 14 [s]Wote wale
wanaovuka, wenye umri wa miaka ishirini
au zaidi, watatoa sadaka kwa BWANA.
15 [t]Matajiri hawatalipa zaidi ya nusu shekeli,
nao maskini hawatatoa pungufu wakati
mnatoa sadaka kwa BWANA kwa kufanya
upatanisho wa nafsi zenu. 16 [u]Utapokea
fedha ya upatanisho kutoka kwa Waisraeli
na uzitumie kwa ajili ya huduma ya Hema
la Kukutania. Itakuwa ni ukumbusho

---

[a]**29:45** Kut 25:8; Hes 35:34; Yn 14:17; Rum 8:10; Mwa 17:7; 2Kor 6:16; Ufu 21:3
[b]**29:46** Kut 6:6; 19:4-6; Kum 5:6; Za 114:1; Hag 2:5; Mwa 17:7; Kut 20:2
[c]**30:1** Kut 40:5, 26; Hes 4:11; 1Fal 6:20; Eze 41:22; Kut 25:6; 37:29; Lk 1:11; Ebr 9:4; Ufu 8:3
[d]**30:2** Kut 27:2; Ufu 9:13
[e]2 Dhiraa moja ni sawa na sentimita 45.
[f]2 Dhiraa mbili ni sawa na sentimita 90.
[g]**30:3** Kut 25:11
[h]**30:4** Kut 25:12
[i]**30:5** Kut 25:13
[j]**30:6** Kut 25:22; 26:34
[k]**30:7** Kut 26:6; 40:27; Hes 3:10; Kum 33:10; 1Sam 2:28; 1Nya 6:49; 2Nya 2:4; 26:18
[l]**30:8** Kut 25:37; 29:42
[m]**30:9** Law 10:1; Hes 16:7, 40
[n]**30:10** Law 16:2; 9:7; 16:18-19; 23:27-28; 25:9; Kut 29:14; Law 4:3; 6:25; 7:7; 8:2; 14; Hes 6:11; Kut 29:42
[o]**30:12** Kut 38:25; Hes 1:2, 49; 4:2, 29; 14:29; 14:29; 26:2; 31:26; 2Sam 24:1; 2Fal 12:4; Kut 38:26; Hes 31:50; Mt 20:28; Hes 14:12; Kum 28:58-61; 2Sam 24:13; 1Fal 8:37
[p]**30:13** Kut 38:24-26; Law 15:15; 27:3; Hes 3:47; 7:13; 18:16; Eze 4:10; 45:12; Mt 17:24
[q]13 Nusu shekeli ni sawa na gramu 6.
[r]13 Gera 20 ni sawa na shekeli moja au gramu 12.
[s]**30:14** Kut 38:26; Hes 14:29; 26:2; 32:11; 2Nya 25:5
[t]**30:15** Mit 22:2; Efe 6:9
[u]**30:16** Kut 38:25-28; 2Nya 24:5; Hes 31:54

kwa Waisraeli mbele za BWANA kufanya
upatanisho kwa ajili ya nafsi zenu."

*Sinia La Kunawia*

17 Kisha BWANA akamwambia Mose,
18 [a]"Tengeneza sinia la shaba lenye kitako
cha shaba kwa ajili ya kunawia. Liweke
kati ya Hema la Kukutania na madhabahu,
kisha uweke maji ndani yake. 19 [b]Aroni
na wanawe watanawa mikono na miguu
yao kwa maji yatokayo katika hilo sinia.
20 [c]Wakati wowote wanapoingia katika
Hema la Kukutania, watanawa kwa maji ili
kwamba wasije wakafa. Pia, wanapokaribia
madhabahu ili kuhudumu kwa kuleta
sadaka zilizotolewa kwa BWANA kwa
moto, 21 [d]watanawa mikono na miguu yao
ili kwamba wasije wakafa. Hii itakuwa
ni amri ya kudumu kwa ajili ya Aroni na
wazao wake kwa vizazi vijavyo."

*Mafuta Ya Upako*

22 [e]Kisha BWANA akamwambia Mose,
23 [f]"Chukua vikolezi bora vifuatavyo: shekeli
500[g] za manemane ya maji, shekeli 250[h]
za mdalasini wenye harufu nzuri, shekeli
250 za miwa yenye harufu nzuri, 24 [i]shekeli
500 za aina nyingine ya mdalasini,
vyote kulingana na shekeli ya mahali
patakatifu, pia hini[j] ya mafuta ya zeituni.
25 [k]Vitengeneze vikolezi hivi kuwa mafuta
matakatifu ya upako yenye harufu nzuri,
kazi ya mtengeneza manukato. Yatakuwa
mafuta matakatifu ya upako. 26 [l]Kisha
yatumie kupaka hilo Hema la Kukutania,
Sanduku la Ushuhuda, 27 meza na vifaa
vyake vyote, kinara cha taa na vifaa vyake
vyote, madhabahu ya kufukizia uvumba,
28 madhabahu ya sadaka ya kuteketezwa
na vyombo vyake vyote na sinia pamoja
na kitako chake. 29 [m]Utaviweka wakfu ili
viwe vitakatifu sana na kila kitakachoigusa
kitakuwa kitakatifu.

30 [n]"Mtie Aroni na wanawe mafuta na
uwaweke wakfu ili waweze kunitumikia
katika kazi ya ukuhani. 31 [o]Waambie
Waisraeli, 'Haya yatakuwa mafuta
matakatifu yangu ya upako kwa vizazi
vijavyo. 32 Usiyamimine juu ya miili ya
wanadamu wala usitengeneze mafuta
ya aina nyingine kwa utaratibu huu. Ni
mafuta matakatifu na ni lazima myaone
kuwa ni matakatifu. 33 [p]Mtu yeyote
atakayetengeneza manukato kama hayo
na yeyote atakayeyamimina juu ya mtu
yeyote ambaye si kuhani atakatiliwa mbali
na watu wake.' "

*Uvumba*

34 [q]Kisha BWANA akamwambia Mose,
"Chukua vikolezi vyenye harufu nzuri
vifuatavyo: natafi, shekelethi, kelbena
na uvumba safi vyote vikiwa na vipimo
sawa, 35 [r]pia tengeneza mchanganyiko
wa uvumba wenye harufu nzuri, kazi ya
mtengeneza manukato. Utiwe chumvi
ili upate kuwa safi na mtakatifu. 36 [s]Saga
baadhi yake kuwa unga na uweke mbele
ya Sanduku la Ushuhuda ndani ya Hema
la Kukutania, mahali ambapo nitakutana
nawe. Itakuwa takatifu sana kwenu.
37 Msitengeneze uvumba mwingine wowote
wa namna hii kwa ajili yenu wenyewe;
uoneni kuwa ni mtakatifu kwa BWANA.
38 Yeyote atakayetengeneza uvumba kama

---

[a]**30:18** Kut 31:9; 35:16; 38:8; 39:39; 40:7, 30; 1Fal 7:38; 2Nya 4:6
[b]**30:19** Kut 40:31-32; Yn 13:10; Kut 29:4; 40:12; Law 8:6; Za 26:6; Ebr 10:22
[c]**30:20** Kut 28:43
[d]**30:21** Kut 27:21; 28:43; 29:42
[e]**30:22** Mwa 43:11; 37:25; Mit 7:17; Wim 4:14; Isa 43:24; Yer 6:20
[f]**30:23** Wim 4:14; Eze 27:22; Za 45:8; Yer 6:20
[g]23 Shekeli 500 ni sawa na kilo 6.
[h]23 Shekeli 250 ni sawa na kilo 3.
[i]**30:24** Za 45:8; Eze 27:19; Kut 29:40
[j]24 Hini moja ni sawa na lita 4.
[k]**30:25** 1Nya 9:30; Kut 37:29; 29:7; 1Sam 9:16; Hes 35:25; Za 133:2
[l]**30:26** Kut 40:9; Law 8:10; Hes 7:1
[m]**30:29** Law 8:10-11; 6:18, 27; Kut 29:37; Mt 23:17
[n]**30:30** Kut 29:7; Law 8:2, 12, 30; 10:7; 16:32; 21:10-12; 1Nya 15:12; Za 133:2; Kut 28:41
[o]**30:31** Kut 29:7, 42
[p]**30:33** Mwa 17:14; Law 7:20, 21
[q]**30:34** Wim 3:6; Kut 25:6; 37:29
[r]**30:35** Kut 25:6
[s]**30:36** Kut 29:37; Law 2:3

huu ili kufurahia harufu yake nzuri lazima
akatiliwe mbali na watu wake.”

### *Bezaleli Na Oholiabu*

**(Kutoka 35:30–36:1)**

31 Ndipo Bwana akamwambia Mose,
2 [a]“Tazama, nimemchagua Bezaleli
mwana wa Uri, mwana wa Huri, wa kabila la
Yuda, 3 [b]nami nimemjaza Roho wa Mungu,
pamoja na ustadi, uwezo na ujuzi katika
aina zote za ufundi, 4 ili kubuni michoro
ya kupendeza katika ufundi wa dhahabu,
fedha na shaba, 5 kuchonga vito na kuvitia
mahali, kufanya ufundi kwa mbao, na
kujishughulisha na aina zote za ufundi.
6 [c]Tena nimemteua Oholiabu mwana wa
Ahisamaki, wa kabila la Dani, ili kumsaidia.
Pia mafundi wote nimewapa ustadi wa
kutengeneza kila kitu nilichokuamuru
wewe: 7 [d]Hema la Kukutania, Sanduku
la Ushuhuda pamoja na kiti cha rehema
juu yake, pia na vifaa vyote vya kwenye
hema, 8 [e]meza na vifaa vyake, kinara
cha taa cha dhahabu safi na vifaa vyake
vyote, madhabahu ya kufukizia uvumba,
9 [f]madhabahu ya sadaka ya kuteketezwa
na vyombo vyake vyote, sinia na kinara
chake, 10 [g]pamoja na mavazi matakatifu
yaliyofumwa ya kuhani Aroni, na mavazi
kwa ajili ya wanawe wakati wanahudumu
katika kazi ya ukuhani, 11 [h]pia mafuta ya
upako na uvumba wenye harufu nzuri kwa
ajili ya Mahali Patakatifu. Watavitengeneza
sawasawa kama vile nilivyokuagiza wewe.”

### *Sabato*

12 Kisha Bwana akamwambia Mose,
13 [i]“Waambie Waisraeli, ‘Ninyi ni lazima
mzishike Sabato zangu. Hii itakuwa ni
ishara kati yangu na ninyi kwa ajili ya
vizazi vijavyo, ili mpate kujua kwamba
Mimi Ndimi Bwana, niwafanyaye ninyi
watakatifu.
14 [j]“ ‘Mtaishika Sabato, kwa sababu ni
takatifu kwenu. Yeyote atakayeinajisi
lazima auawe, yeyote atakayefanya kazi
siku hiyo lazima akafie mbali na watu wake.
15 [k]Kwa siku sita, mtafanya kazi, lakini siku
ya saba ni Sabato ya kupumzika, takatifu
kwa Bwana. Yeyote afanyaye kazi yoyote
siku ya Sabato ni lazima auawe. 16 [l]Waisraeli
wataishika Sabato, kuiadhimisha kwa vizazi
vijavyo kuwa Agano la milele. 17 [m]Itakuwa
ishara kati yangu na Waisraeli milele,
kwa kuwa kwa muda wa siku sita Bwana
aliumba mbingu na dunia, na siku ya saba
akaacha kufanya kazi, akapumzika.’ ”
18 [n]Bwana alipomaliza kusema na Mose
juu ya Mlima Sinai, Mungu akampa vile
vibao viwili vya Ushuhuda, vibao vya mawe
vilivyoandikwa kwa kidole cha Mungu.

### *Ndama Wa Dhahabu*

**(Kumbukumbu 9:6-29)**

32 [o]Watu walipoona kuwa Mose
amekawia sana kushuka kutoka
mlimani, walimkusanyikia Aroni na
kumwambia, “Njoo, tutengenezee miungu
itakayotutangulia. Kwa maana huyu jamaa
yetu Mose aliyetupandisha kutoka Misri,
hatujui jambo lililompata.”
2 [p]Aroni akawajibu, “Vueni vipuli vya
dhahabu ambavyo wake zenu, wana wenu
na binti zenu wamevaa, mkaniletee.” 3 Kwa
hiyo watu wote wakavua vipuli vyao,

---

[a]**31:2** Kut 36:1-2; 37:1; 38:22; 1Nya 21:20; 2Nya 1:5; Kut 17:10
[b]**31:3** Kut 28:3; 1Fal 7:14; 1Kor 12:4; Kut 35:31; Isa 28:26
[c]**31:6** Kut 36:1-2; 38:23; 1Fal 7:14; 2Nya 2:14
[d]**31:7** Kut 36:8-38; 37:1-6; 40:20
[e]**31:8** Kut 37:10-24; Law 24:4; Kut 37:25-28
[f]**31:9** Kut 38:3; Hes 4:14; Kut 30:18
[g]**31:10** Kut 28:2; 39:1, 41
[h]**31:11** Kut 30:22-32; 37:29; 25:6-9
[i]**31:13** Kut 20:8; Isa 56:4; Eze 20:12, 20; Kut 29:42; Law 11:44; 20:8; Eze 37:28
[j]**31:14** Kut 35:2; Hes 15:32-36
[k]**31:15** Kut 20:8-11; 35:2; Law 16:29; 23:3; Hes 29:7; Mwa 2:3
[l]**31:16** Kut 20:8
[m]**31:17** Mwa 2:2-3; Kut 20:9; Isa 56:2; 58:13; 66:23; Yer 17:21-22; Eze 20:12, 20
[n]**31:18** Kut 19:11; 24:12; 2Kor 3:3; Ebr 9:4; Kut 32:15-16; 34:1; 28; Kum 4:30; 9:10
[o]**32:1** Mwa 7:4; Kum 9:9-12; Kut 13:21; 24:18; Mdo 7:40
[p]**32:2** Kut 35:22; Amu 8:24-27

wakavileta kwa Aroni. 4 [a]Akavichukua vile
vitu walivyomkabidhi, akavifanyiza kwa
kusubu sanamu yenye umbo la ndama,
akaichonga kwa kutumia chombo. Kisha
wakasema, "Hii ndiyo miungu yenu, ee
Israeli, iliyowapandisha kutoka Misri."
5 [b]Aroni alipoona hili, akajenga
madhabahu mbele ya yule ndama na
kutangaza, "Kesho kutakuwa na sikukuu
kwa BWANA." 6 [c]Kwa hiyo siku iliyofuata
watu wakaamka asubuhi na mapema na
kutoa sadaka za kuteketeza na sadaka za
amani. Baadaye watu wakaketi kula na
kunywa, nao wakasimama, wakajizamisha
katika sherehe.
7 [d]Kisha BWANA akamwambia Mose,
"Shuka, kwa sababu watu wako, uliowatoa
Misri, wamepotoka. 8 [e]Wamekuwa wepesi
kugeuka na kuacha niliyowaamuru, na
wamejitengenezea sanamu ya kuyeyusha
yenye umbo la ndama. Wameisujudia na
kuitolea dhabihu, nao wamesema, 'Hii ndiyo
miungu yenu, ee Israeli iliyokupandisha
kutoka Misri.' "
9 [f]BWANA akamwambia Mose, "Nimeona
watu hawa, nao ni watu wenye shingo
ngumu. 10 [g]Sasa niache ili hasira yangu
ipate kuwaka dhidi yao, nami nipate
kuwaangamiza. Kisha nitakufanya wewe
kuwa taifa kubwa."
11 [h]Lakini Mose akamsihi BWANA Mungu
wake, akasema, "Ee BWANA, kwa nini
hasira yako iwake dhidi ya watu wako, wale
uliowatoa Misri kwa uweza mkuu na mkono
wenye nguvu? 12 [i]Kwa nini Wamisri waseme,
'Ni kwa nia mbaya aliwatoa Misri, ili awaue
milimani na kuwafuta usoni mwa dunia'?
Achilia mbali hasira yako kali, waonee
huruma na usilete maafa juu ya watu wako.
13 [j]Wakumbuke watumishi wako Abrahamu,
Isaki na Israeli, ambao uliwaapia kwa
nafsi yako mwenyewe: 'Nitawafanya uzao
wako kuwa wengi kama nyota za angani,
nami nitawapa wazao wako nchi hii yote
ambayo niliwaahidia, nayo itakuwa urithi
wao milele.' " 14 [k]Kisha BWANA akawaonea
huruma, wala hakuleta juu ya watu wake
maafa aliyokuwa amekusudia.
15 [l]Mose akageuka, akashuka kutoka
mlimani akiwa na vibao viwili vya
Ushuhuda mikononi mwake. Vilikuwa
vimeandikwa pande zote mbili, mbele na
nyuma. 16 [m]Vibao hivyo vilikuwa kazi ya
Mungu; maandishi yalikuwa mwandiko wa
Mungu, yaliyochorwa kama muhuri juu ya
vibao.
17 [n]Yoshua aliposikia sauti za watu
wakipiga kelele, akamwambia Mose, "Kuna
sauti ya vita kambini."
18 Mose akajibu:

"Si sauti ya ushindi,
wala si sauti ya kushindwa;
ni sauti ya kuimba ninayosikia."

---

[a]**32:4** Kut 20:23; Amu 17:3-4; Isa 30:22; Kum 9:16; Neh 9:18; Za 106:19; Mdo 7:41; Kut 20:23; Isa 42:17; 1Fal 12:28; 14:9; 2Fal 10:29; 17:16; 2Nya 13:8; Hos 8:6; 10:5
[b]**32:5** Law 23:2, 37; 2Fal 10:20; Yoe 2:15
[c]**32:6** Kut 20:24; 34:15; Law 3:1; 4:10; 6:12; 9:4; 22:21; Hes 6:14; 25:2; Kum 27:7; Amu 20:26; Eze 43:27; Mdo 7:14; Amu 19:4; Rut 3:3; 1Sam 1:9; 2Sam 11; 11; 1Fal 13:23; 18:42; Neh 8:12; Mhu 5:18; Yer 16:8; 1Kor 10:7
[d]**32:7** Kut 33:1; Mwa 6:11-12; Kut 20:8
[e]**32:8** Yer 7:26; 16:12; Mal 2:8; 3:7; Kut 20:4; 22:20; 1Fal 12:28; Eze 23:8
[f]**32:9** Kut 33:3-5; 34:9; Kum 9:6, 13; 10:16; 31:27; Amu 2:19; 2Fal 17:14; 2Nya 30:8; 36:13; Neh 9:16; Za 78:8; Mit 29:1; Isa 46:12; 48:4; Yer 7:26; Eze 2:4; Hos 4:16; Mdo 7:51
[g]**32:10** 1Sam 2:25; Yer 11:14; 7:16; 14:11; Kut 22:24; 33:3-5; Hes 16:21; Kum 9:14-19; Za 106:22; Yer 14:12; Eze 20:13; Hes 14:12; Dan 9:14
[h]**32:11** Kum 9:18; 2Sam 21:1; 2Nya 15:2; Za 9:10; 34:4; 106:23; Isa 9:13; Yer 15:1; Kum 9:26; 1Sam 7:9; Neh 1:10; Za 136:12
[i]**32:12** Hes 14:13-16; Kum 9:28; Kut 33:13
[j]**32:13** Kut 2:24; 33:14; Mwa 22:16; Ebr 6:13; Mwa 15:5; 22:17; 12:7; 26:4
[k]**32:14** Kum 9:19; 1Sam 15:11; 2Sam 24:16; 1Fal 21:29; 1Nya 21:15; Za 106:45; Yer 18:8; 26:3; Amo 7:3; Yn 3:10
[l]**32:15** Kut 31:18; 19:18; Ebr 9:4; Kut 34:4, 29; Kum 9:15; 2Kor 3:3
[m]**32:16** Kut 24:12; 31:18
[n]**32:17** Kut 17:9; 31:18

19 [a]Mose alipoikaribia kambi na kuona yule
ndama na ile michezo, hasira yake ikawaka,
akatupa vile vibao vilivyokuwa mikononi
mwake, akavipasua vipande vipande pale
chini ya mlima. 20 [b]Kisha akamchukua yule
ndama waliokuwa wamemtengeneza na
kumchoma kwenye moto, kisha akamsaga
kuwa unga, akanyunyiza kwenye maji na
kuwafanya Waisraeli wanywe.
21 Mose akamwambia Aroni, "Watu hawa
walikufanyia nini, hata ukawaongoza
kufanya dhambi kubwa hivyo?"
22 [c]Aroni akamwambia, "Usikasirike
bwana wangu. Unajua jinsi watu
hawa walivyo tayari kwa maovu.
23 [d]Wao waliniambia, 'Tufanyie miungu
itakayotuongoza. Kwa kuwa huyu jamaa
yetu Mose aliyetupandisha kutoka Misri,
hatufahamu yaliyompata.' 24 Kwa hiyo
nikawaambia, 'Yeyote aliye na kito chochote
cha dhahabu avue.' Kisha wakanipa hiyo
dhahabu, nami nikaitupa motoni, akatokea
huyu ndama!"
25 [e]Mose akaona kuwa watu wameasi,
kwa kuwa Aroni alikuwa amewaacha
waasi, na hivyo kuwa kichekesho kwa adui
zao. 26 Kwa hiyo Mose akasimama kwenye
ingilio la kambi, akasema, "Yeyote aliye
upande wa BWANA, aje upande wangu."
Walawi wote wakamjia.
27 [f]Ndipo alipowaambia, "Hili ndilo
BWANA, Mungu wa Israeli asemalo: 'Kila
mmoja wenu ajifunge upanga wake kiunoni
aende huku na huko kambi yote mwisho
hadi mwisho mwingine, kila mmoja
amuue ndugu yake, na rafiki yake na
jirani yake.' " 28 Walawi wakafanya kama
Mose alivyoamuru, siku ile wakafa watu
wapatao 3,000. 29 Kisha Mose akasema,
"Leo mmewekwa wakfu kwa BWANA, kwa
kuwa mlikuwa kinyume na wana wenu
wenyewe na ndugu zenu, naye Mungu
amewabariki leo."
30 [g]Siku iliyofuata Mose akawaambia
watu, "Mmefanya dhambi kubwa. Lakini
sasa nitapanda juu kwa BWANA, labda
nitaweza kufanya upatanisho kwa ajili ya
dhambi yenu."
31 [h]Hivyo Mose akarudi kwa BWANA
na kumwambia, "Lo! Hawa watu
wamefanya dhambi kubwa namna gani!
Wamejitengenezea miungu ya dhahabu.
32 [i]Lakini sasa nakusihi, wasamehe dhambi
yao; lakini kama sivyo, basi nifute kutoka
kwenye kitabu ulichoandika."
33 [j]BWANA akamjibu Mose, "Yeyote
aliyenitenda dhambi ndiye nitakayemfuta
kutoka kwenye kitabu changu. 34 [k]Sasa
nenda, uongoze hao watu mpaka mahali
nilipokuambia, naye malaika wangu
atakutangulia. Pamoja na hayo, wakati
utakapofika wa mimi kuwaadhibu,
nitawaadhibu kwa ajili ya dhambi yao."
35 [l]Ndipo BWANA akawapiga watu kwa
ugonjwa wa tauni kwa sababu ya yale
waliyoyafanya kwa ndama yule ambaye
alitengenezwa na Aroni.

### *Amri Ya Kuondoka Sinai*

33 [m]Kisha BWANA akamwambia Mose,
"Ondoka mahali hapa, wewe pamoja
na hao watu uliowapandisha kutoka
Misri, mpande mpaka nchi niliyomwahidi
Abrahamu, Isaki na Yakobo kwa kiapo,
nikisema, 'Nitawapa wazao wenu nchi hii.'
2 [n]Nitamtuma malaika mbele yenu, naye

---

[a]**32:19** Kum 9:16; 1Kor 10:7; Ezr 9:3; Za 119:53, 158; Kut 34:1; Kum 9:17
[b]**32:20** Kut 7:25; 12:3; Yos 7:1; 2Fal 23:6; 1Nya 14:12; 2Nya 34:7; Mik 1:7; Kum 9:21
[c]**32:22** Mwa 18:30; Kum 9:24; 28:20; 2Fal 21:15; Ezr 9:13; Neh 9:28; Yer 4:4; 44:3; Eze 6:9
[d]**32:23** Mdo 7:40
[e]**32:25** Mwa 38:23
[f]**32:27** Hes 25:3-5; Kum 33:9; Eze 9:5
[g]**32:30** 1Sam 12:20; Za 25:11; 85:2; Law 4:20; 5:6-13; 6:7; Hes 25:13
[h]**32:31** Kut 34:9; 9:18; 20:23
[i]**32:32** Hes 14:19; Rum 9:3; Za 69:28; Eze 13:9; Dan 7:10; 12:1; Mal 3:16; Lk 10:20; Efe 4:3
[j]**32:33** Kut 17:14; Ay 21:20; Ufu 3:5; Za 9:5
[k]**32:34** Kut 15:17; 3:17; 14:19; Mwa 50:19; Kum 32:35; Za 89:32; 94:23; 99:8; 109:20; Isa 27:1; Yer 5:9; 11:22; 23:20; 44:13, 29; Hos 12:2; Rum 2:5-6
[l]**32:35** 2Sam 12:9
[m]**33:1** Kut 13:11; Hes 14:23; Ebr 6:13; Mwa 12:7
[n]**33:2** Kut 14:19; 23:28; Kum 7:22; Yos 24:11

atawafukuza Wakanaani, Waamori, Wahiti,
Waperizi, Wahivi na Wayebusi. 3 [a]Pandeni
mwende katika nchi itiririkayo maziwa
na asali. Lakini mimi sitakwenda pamoja
nanyi, kwa sababu ninyi ni watu wenye
shingo ngumu, nisije nikawaangamiza
njiani."
4 [b]Watu waliposikia habari hizo za
huzuni, wakaanza kuomboleza wala hakuna
mtu aliyevaa mapambo yoyote. 5 [c]Kwa
kuwa BWANA alikuwa amemwambia Mose,
"Waambie Waisraeli, 'Ninyi ni watu wenye
shingo ngumu. Kama ningefuatana nanyi
hata kwa muda mfupi, ningewaangamiza.
Sasa vueni mapambo yenu, nami nitaamua
nitakalowatendea.' " 6 Hivyo Waisraeli
wakavua mapambo yao katika Mlima wa
Horebu.

*Hema La Kukutania*

7 [d]Basi Mose alikuwa na desturi ya
kuchukua hema na kuliweka wakfu nje
ya kambi umbali kiasi, akaliita "Hema
la Kukutania." Kila aliyekuwa akiulizia
shauri kwa BWANA, angelikwenda katika
Hema la Kukutania nje ya kambi. 8 [e]Wakati
wowote Mose alipokwenda kwenye Hema,
watu wote waliinuka na kusimama kwenye
maingilio ya mahema yao, wakimwangalia
Mose mpaka aingie kwenye Hema. 9 [f]Kila
mara Mose alipoingia ndani ya hema,
nguzo ya wingu ingeshuka chini na kukaa
kwenye ingilio, wakati Mungu akizungumza
na Mose. 10 Kila mara watu walipoona
hiyo nguzo ya wingu ikiwa imesimama
kwenye ingilio la hema, wote walisimama
wakaabudu, kila mmoja kwenye ingilio
la hema lake. 11 [g]BWANA angezungumza
na Mose uso kwa uso, kama vile mtu
azungumzavyo na rafiki yake. Kisha Mose
angerudi kambini, lakini msaidizi wake
kijana Yoshua mwana wa Nuni hakuondoka
mle Hemani.

*Mose Na Utukufu Wa BWANA*

12 [h]Mose akamwambia BWANA,
"Umekuwa ukiniambia, 'Ongoza watu
hawa,' lakini hujanifahamisha ni nani
utakayemtuma pamoja nami. Umesema,
'Ninakujua wewe kwa jina lako, nawe
umepata kibali mbele zangu.' 13 [i]Ikiwa
umependezwa nami, nifundishe njia zako
ili nipate kukujua, nami nizidi kupata kibali
mbele zako. Kumbuka kuwa taifa hili ni
watu wako."
14 [j]BWANA akajibu, "Uso wangu
utakwenda pamoja nawe, nami nitakupa
raha."
15 [k]Kisha Mose akamwambia, "Kama Uso
wako hauendi pamoja nasi, usituondoe
hapa. 16 [l]Mtu yeyote atajuaje kuwa mimi
pamoja na watu wako tumepata kibali
mbele zako, usipokwenda pamoja nasi? Ni
nini kingine kitakachoweza kututofautisha
mimi na watu wako miongoni mwa watu
wengine wote walio katika uso wa dunia?"
17 [m]BWANA akamwambia Mose,
"Nitakufanyia jambo lile uliloomba,
kwa sababu ninapendezwa nawe, nami
ninakujua kwa jina lako."
18 [n]Kisha Mose akasema, "Basi nionyeshe
utukufu wako."

---

[a]**33:3** Kut 3:8; 32:9-10; Mdo 7:51; Kum 9:6
[b]**33:4** Hes 14:39; Ezr 9:3; Es 4:1; Za 119:53; 2Sam 19:24
[c]**33:5** Kut 32:9-10
[d]**33:7** Kut 27:21; Mwa 25:22; 1Fal 22:5; Kut 29:42-43; 2Sam 21:1
[e]**33:8** Hes 16:27
[f]**33:9** Kut 13:21; 19:9; Kum 31:15; 1Kor 10:1; Kut 29:42; 31:18; Za 99:7
[g]**33:11** Hes 12:8; Kum 5:4; 34:10; Kut 17:9; Mwa 32:30; Kut 24:13
[h]**33:12** Kut 3:10; 15:17; Isa 43:1; 45:3; 49:1; Yn 10:14-15; 2Tim 2:19; Mwa 6:8
[i]**33:13** Za 25:4; 27:11; 51:13; 86:11; 103:7; 143:8; Kut 3:7; Kum 9:26-29; Za 77:15; Yoe 2:17
[j]**33:14** Kut 13:21; Kum 4:37; Isa 63:9; Hag 1:13; 2:4; Kum 12:9-10; 25:19; Yos 1:13; 11:23; 21:44; 22:4; 1Fal 8:56; Isa 63:14; Yer 31:2; Mt 11:28; Ebr 4:1-11
[k]**33:15** Kut 34:9; 2Fal 13:23; 17:18; 23:27; 24:20; Za 51:11; 80:3, 7; Yer 7:15; 52
[l]**33:16** Kut 34:5; 40:34-35; Hes 9:15; 14:14; Kut 34:10; Law 20:24-26; Hes 23:9; Kum 4:7, 32, 34; 32:9; 33:28
[m]**33:17** Kut 34:28; Kum 9:18, 25; 10:10; Yak 5:16; Mwa 6:8
[n]**33:18** Kut 16:7; Yn 1:12; 12:41; 1Tim 6:16; Ufu 15:8

19 [a]Ndipo BWANA akasema, “Nitapitisha
wema wangu wote mbele yako, nami
nitalitangaza Jina langu, BWANA, mbele ya
uso wako. Nitamrehemu yeye nimrehemuye,
na pia nitamhurumia yeye nimhurumiaye.”
20 [b]Lakini Mungu akasema, “Hutaweza
kuuona uso wangu, kwa kuwa hakuna mtu
yeyote awezaye kuniona akaishi.”
21 Kisha BWANA akasema, “Kuna mahali
karibu nami ambapo unaweza kusimama juu
ya mwamba. 22 [c]Utukufu wangu unapopita,
nitakuweka gengeni kwenye mwamba na
kukufunika kwa mkono wangu mpaka
nitakapokwisha kupita. 23 Kisha nitaondoa
mkono wangu nawe utaona mgongo wangu;
lakini kamwe uso wangu hautaonekana.”

*Vibao Vipya Vya Mawe*

**(Kumbukumbu 10:1-5)**

34 [d]BWANA akamwambia Mose, “Chonga
vibao viwili vya mawe kama vile
vya kwanza, nami nitaandika juu yake
maneno yale yaliyokuwa kwenye vile
vibao vya kwanza, ulivyovivunja. 2 [e]Uwe
tayari asubuhi, kisha upande juu ya Mlima
Sinai. Uje mbele zangu kukutana nami huko
juu ya mlima. 3 [f]Mtu yeyote asije pamoja
nawe, wala asionekane mtu popote juu ya
mlima, wala kondoo na mbuzi au ng’ombe
wasilishe karibu mbele ya huo mlima.”
4 [g]Kwa hiyo Mose akachonga vibao
viwili vya mawe kama vile vya kwanza,
naye akapanda juu ya Mlima Sinai asubuhi
na mapema, kama BWANA alivyokuwa
amemwagiza, akachukua vile vibao viwili
vya mawe mikononi mwake. 5 [h]Kisha
BWANA akashuka katika wingu akasimama
pamoja naye huko, akalitangaza jina
lake, BWANA. 6 [i]BWANA akapita mbele
ya Mose, akitangaza, “BWANA, BWANA,
Mungu mwenye huruma na neema, asiye
mwepesi wa hasira, mwingi wa upendo
na uaminifu, 7 [j]akidumisha upendo kwa
maelfu, pia akisamehe uovu, uasi na
dhambi. Lakini haachi kuadhibu mwenye
hatia; huwaadhibu watoto na watoto wao
kwa ajili ya dhambi ya baba zao hata katika
kizazi cha tatu na cha nne.”
8 Mara Mose akasujudu na kuabudu.
9 [k]Mose akasema, “Ee BWANA, kama
nimepata kibali mbele zako, basi BWANA
uende pamoja nasi. Ingawa watu hawa ni
wenye shingo ngumu, samehe uovu wetu na
dhambi yetu, tuchukue kuwa urithi wako.”

*Kufanya Agano Upya*

**(Kutoka 23:14-19; Kumbukumbu 7:1-5; 16:1-17)**

10 [l]Kisha BWANA akasema: “Tazama
ninafanya Agano mbele ya watu wako
wote. Mbele ya watu wako wote nitafanya
maajabu ambayo hayajafanyika katika
taifa lolote katika ulimwengu wote.
Watu wale mnaoishi miongoni mwao
wataona jinsi ilivyo ya kushangaza ile
kazi nitakayowafanyia mimi BWANA
wenu. 11 [m]Tii yale ninayokuamuru leo.
Tazama nawafukuza mbele yako Waamori,
Wakanaani, Wahiti, Waperizi, Wahivi na
Wayebusi. 12 [n]Uwe mwangalifu, usifanye
agano na wale wanaokaa katika nchi ile

[a]**33:19** 1Fal 19:11; Kut 6:3; 34:5-7; Rum 9:15
[b]**33:20** Mwa 16:13; Kut 3:6; Kum 5:26; Yn 1:18; Isa 6:5
[c]**33:22** Mwa 49:24; 1Fal 19:9; Za 27:5; 31:20; 62:7; 91:1; Isa 2:21; Yer 4:29; Isa 49:2; 51:16; Za 91:4
[d]**34:1** Kut 24:12; Kum 10:2-4; Kut 32:19
[e]**34:2** Kut 19:11
[f]**34:3** Kut 19:13
[g]**34:4** Kum 10:3; Kut 32:15
[h]**34:5** Kut 13:21; 19:9; 6:3; 33:19
[i]**34:6** Kut 22:27; Hes 14:20; Za 86:15; 78:18; Rum 2:4; Yer 15:15; Mwa 19:16; Za 61:7; Yoe 2:13; Mao 3:23; Yak 5:11; Hes 14:18
[j]**34:7** Kut 20:5-6; Kum 5:10; 1Fal 8:30; Za 86:5; 103:3; 130:4-8; Isa 43:25; Dan 9:9; 1Yn 1:9; Kut 23:7; Yos 24:19; Ay 7:20-21; 10:14; Mik 6:1-16; Nah 1:3
[k]**34:9** Kut 33:13-15; Hes 11:15; Kut 32:9; Hes 14:19; 1Fal 8:30; 2Nya 6:21; Za 19:12; 25:11; Yer 33:8; Hos 14:2; Kut 6:7; 19:5; Kum 4:20; 7:6; 9:26-29; 14:2; 26:18; 32:9; 1Sam 10:1; 2Sam 14:16; 1Fal 8:51, 53; Za 28:9; 33:12; 74:2; 79:1; 94:14; 106:5, 40; Isa 19:25; 63:17; Yer 10:16; 51:19; Mik 7:18; Zek 2:12
[l]**34:10** Mwa 6:18; 9:15; 15:15, 18; Kum 5:2-3; Kut 3:20; 33:16
[m]**34:11** Kum 6:25; Yos 11:15; Kut 23:28; 32:2
[n]**34:12** Amu 2:2; Kut 10:7; 23:32-33

unayoiendea, la sivyo watakuwa mtego
katikati yako. 13 [a]Bomoa madhabahu yao,
vunja mawe yao ya kuabudia na ukatekate
nguzo zao za Ashera. 14 [b]Usiabudu mungu
mwingine, kwa kuwa Bwana, ambaye jina
lake ni Wivu, ni Mungu mwenye wivu.
15 [cd]“Uwe mwangalifu usifanye agano
na wale watu wanaoishi katika nchi, kwa
maana wakati wanapojifanyia ukahaba
kwa miungu yao na kuwatolea kafara,
watakualika wewe nawe utakula sadaka za
matambiko yao. 16 [e]Unapowachagua baadhi
ya binti zao kuwa wake wa wana wenu
na binti hao wakajifanyia ukahaba kwa
miungu yao, watawaongoza wana wenu
kufanya vivyo hivyo.
17 [f]“Usijifanyie sanamu za kusubu.
18 [g]“Utaadhimisha Sikukuu ya Mikate
Isiyotiwa Chachu. Kwa siku saba
mtakula mikate isiyotiwa chachu, kama
nilivyokuamuru. Fanya hivi kwa wakati
ulioamriwa, katika mwezi wa Abibu, ndio
mwezi wa nne, kwa kuwa katika mwezi
huo ndipo wewe ulipotoka Misri.
19 [h]“Mzaliwa wa kwanza wa kila tumbo
ni mali yangu, pamoja na wazaliwa wa
kwanza wote wa kiume wa mifugo yako,
ikiwa ni wa ng’ombe au wa kondoo au
mbuzi. 20 [i]Utakomboa mzaliwa wa kwanza
wa punda kwa mwana-kondoo, lakini
kama humkomboi, utavunja shingo yake.
Utakomboa wazaliwa wako wa kwanza
wote wa kiume.
“Mtu yeyote asije mbele zangu mikono
mitupu.
21 [j]“Kwa siku sita utafanya kazi, lakini
siku ya saba utapumzika, hata ikiwa ni
majira ya kulima au ya kuvuna lazima
upumzike.
22 [k]“Utaadhimisha Sikukuu ya Majuma
kwa malimbuko ya mavuno ya ngano, na
Sikukuu ya Mavuno mwishoni mwa mwaka.
23 [l]Mara tatu kwa mwaka wanaume wako
wote watakuja mbele za Bwana Mwenyezi,
Mungu wa Israeli. 24 [m]Nitawafukuza mataifa
mbele yako na kupanua mipaka ya nchi yako,
wala hakuna mtu yeyote atakayeitamani
nchi yako wakati unapokwenda mara tatu
kila mwaka kuonana na Bwana Mungu
wako.
25 [n]“Usinitolee damu ya dhabihu pamoja
na kitu chochote chenye chachu, wala
usibakize dhabihu yoyote ya Sikukuu ya
Pasaka mpaka asubuhi.
26 [o]“Leta matunda ya kwanza yaliyo
bora zaidi ya ardhi yako katika nyumba
ya Bwana Mungu wako.
“Usimchemshe mwana-mbuzi katika
maziwa ya mama yake.”
27 [p]Kisha Bwana akamwambia Mose,
“Andika maneno haya, kwa maana
kulingana na maneno haya, nimefanya
Agano na wewe pamoja na Israeli.” 28 [q]Mose
alikuwa huko pamoja na Bwana kwa siku
arobaini usiku na mchana bila kula chakula
wala kunywa maji. Naye akaandika juu ya

---

[a]**34:13** Kut 23:24; Hes 33:52; Kum 7:5; 12:3; Amu 6:26; 1Fal 15:13; 2Nya 15:16; 17:6; 34:3-4; Mik 5:4
[b]**34:14** Kut 20:3-4; Isa 9:6; Kum 4:24
[c]**34:15** Law 17:7; Hes 25:2; Kum 32:17; Za 106:37; Law 27:29; Kum 13:5; 17:2-5; 18:20; 2Nya 15:13
[d]**34:15** Kum 23:6; Ezr 9:12; Kut 22:20; 32:8; Kum 31:16; Amu 2:17; 2Nya 17:8; 1Nya 17:8; 5:25; 2Nya 11:15; Amo 2:4; Kut 32:6; 1Kor 8:4
[e]**34:16** Kum 7:3; 17:17; Yos 23:12; Amu 3:6; 14:2-3; 1Fal 11:1-2; 16:31; Ezr 9:2; 10:3; Neh 10:30; 13:25-26; Kum 7:4; 12:31; 20:18; 1Fal 11:4; 2Fal 21:3-15; Za 106:34-41; Mal 2:11
[f]**34:17** Kut 20:4; 32:8
[g]**34:18** Kut 12:17; Mt 26:17; Lk 22:1; Mdo 12; Kut 12:15; 12:2
[h]**34:19** Kut 13:2
[i]**34:20** Kut 13:13; 13:2; 22:29; Kum 16:16; Eze 46:9
[j]**34:21** Mwa 2:2-3; Neh 13:15; Isa 56:2; 58; 13; Lk 13:14
[k]**34:22** Kut 23:19; Law 2:12-14; 7:13; 23:10, 17; Hes 28:26; Kut 23:14-16; 34:23
[l]**34:23** Kut 23:14
[m]**34:24** Kut 23:28; Kum 12:20; 19:8; Ay 12:23; Za 78:55
[n]**34:25** Kut 23:18; 12:8-10
[o]**34:26** Kut 22:29; Hes 18:12; Kut 23:19
[p]**34:27** Kut 17:14; Mwa 6:18; 15:18; Kut 24:4; Kum 31:9; Isa 30:8
[q]**34:28** Mwa 7:4; Mt 4:2; Lk 4:2; Kum 9:9, 18; Kut 24:18; Ezr 10:6; Kut 31:18; Kum 4:13; 10:4

vibao maneno ya Agano, yaani zile Amri Kumi.

*Mng'ao Wa Uso Wa Mose*

29 [a]Mose alipoteremka kutoka Mlima Sinai
akiwa na vile vibao viwili vya Ushuhuda
mikononi mwake, hakujua kuwa uso wake
ulikuwa uking'aa, kwa sababu alikuwa
amezungumza na BWANA. 30 Aroni na
Waisraeli wote walipomwona Mose, kuwa
uso wake unang'aa, waliogopa kumkaribia.
31 [b]Lakini Mose akawaita, kwa hiyo Aroni na
viongozi wote wa jumuiya wakarudi, naye
akazungumza nao. 32 [c]Baadaye Waisraeli
wote wakamkaribia, naye akawapa amri
zote BWANA alizompa katika Mlima wa
Sinai.
33 [d]Mose alipomaliza kuzungumza nao,
akaweka utaji kwenye uso wake. 34 Lakini
kila wakati Mose alipoingia mbele za
BWANA kuzungumza naye, aliondoa ule
utaji mpaka alipotoka nje. Naye alipotoka
nje na kuwaambia Waisraeli lile ambalo
ameagizwa, 35 waliona kuwa uso wake
unang'aa. Kisha Mose angeliweka tena
utaji juu ya uso wake mpaka alipokwenda
kuzungumza na BWANA.

*Masharti Ya Sabato*

35 [e]Mose akakusanya jumuiya yote ya
Waisraeli na kuwaambia, "Haya ndiyo
mambo ambayo BWANA amewaamuru
ninyi mfanye: 2 [f]Kwa siku sita, mtafanya
kazi, lakini siku ya saba itakuwa takatifu
kwenu, Sabato ya kupumzika kwa BWANA.
Yeyote atakayefanya kazi yoyote siku hiyo
ni lazima auawe. 3 [g]Msiwashe moto mahali
popote katika makazi yenu siku ya Sabato."

*Vifaa Kwa Ajili Ya Maskani Ya Mungu*

**(Kutoka 25:1-9)**

4 [h]Mose akaiambia jumuiya yote ya
Waisraeli, "Hili ndilo BWANA aliloamuru:
5 [i]Toeni sadaka kwa BWANA kutoka mali
mliyo nayo. Kila mmoja aliye na moyo
wa kupenda atamletea BWANA sadaka
ya dhahabu, fedha na shaba; 6 nyuzi za
rangi ya buluu, za zambarau, za rangi
nyekundu na kitani safi; singa za mbuzi;
7 ngozi za kondoo dume zilizopakwa rangi
nyekundu, na ngozi za pomboo;[j] mbao za
mshita; 8 [k]mafuta ya zeituni kwa ajili ya
taa; vikolezi kwa ajili ya mafuta ya upako,
pamoja na uvumba wa harufu nzuri; 9 vito
vya shohamu, na vito vingine vya thamani
vya kuweka kwenye kisibau na kile kifuko
cha kifuani.
10 [l]"Wote wenye ujuzi miongoni mwenu
inawapasa kuja na kutengeneza kila kitu
BWANA alichoamuru: 11 [m]Maskani pamoja
na hema lake na kifuniko chake, vibanio,
mihimili, mataruma, nguzo na vitako;
12 [n]Sanduku la Agano pamoja na mipiko
yake, kifuniko cha kiti cha rehema na
pazia linalokizuia; 13 [o]meza na mipiko yake
pamoja na vyombo vyake vyote, mikate ya
Wonyesho; 14 [p]kinara cha taa kwa ajili ya
mwanga pamoja na vifaa vyake vyote, taa na
mafuta kwa ajili ya mwanga; 15 [q]madhabahu
ya kufukiza uvumba pamoja na mipiko
yake, mafuta ya upako na uvumba wenye
harufu nzuri; pazia la mlangoni mahali pa
kuingilia ndani ya maskani; 16 [r]madhabahu
ya sadaka za kuteketeza pamoja na wavu
wake wa shaba, mipiko yake pamoja

[a]**34:29** Kut 19:11; 32:15; Za 34:5; Isa 60:5; Mt 17:2; 2Kor 3:7, 13
[b]**34:31** Kut 16:22
[c]**34:32** Kut 21:1; 35:1-4
[d]**34:33** 2Kor 3:13
[e]**35:1** Kut 34:32
[f]**35:2** Law 23:3; Mwa 2:3; Kut 34:21; Kum 5:13-14; Kut 31:14, 15; Hes 15:32; Lk 13:14
[g]**35:3** Kut 16:23
[h]**35:4** Kut 25:1, 2
[i]**35:5** Kut 25:2; 2Kor 9:7
[j]7 *Pomboo* hapa ina maana ya mnyama mwenye ngozi laini aishiye kwenye milima yenye misitu, au pengine nguva au sili.
[k]**35:8** Kut 25:6
[l]**35:10** Kut 31:6; 39:43; 1Fal 7:14; Isa 28:26
[m]**35:11** Kut 26:1-37; 36:8-38; Mdo 7:44, 45; Ebr 8:2, 5; 9:2-11; Ufu 21:3
[n]**35:12** Kut 25:10-22; 37:1-9; 26:33
[o]**35:13** Kut 25:23-30; 37:10-16
[p]**35:14** Kut 25:31
[q]**35:15** Kut 30:1-6; 37:26-28; 30:34-38; 26:36; 1Sam 2:28; 1Nya 23:13; 2Nya 29:11; Lk 1:9
[r]**35:16** Kut 27:1-8; 38:1-7; 30:18

na vyombo vyake vyote; sinia la shaba
pamoja na tako lake; 17 [a]pazia la eneo la
ua pamoja na nguzo zake na vitako vyake,
pazia la ingilio la kwenye ua; 18 [b]vigingi vya
hema kwa ajili ya maskani pamoja na ua
na kamba zake; 19 [c]mavazi yaliyofumwa
yanayovaliwa wakati wa huduma katika
mahali patakatifu, yaani mavazi matakatifu
kwa ajili ya kuhani Aroni, na mavazi
kwa ajili ya wanawe watakapokuwa
wakihudumu katika kazi ya ukuhani."

20 Ndipo jumuiya yote ya Waisraeli
ilipoondoka mbele ya Mose, 21 [d]na kila
mmoja aliyependa na ambaye moyo wake
ulimsukuma alikuja na kuleta sadaka kwa
BWANA, kwa ajili ya kazi katika Hema
la Kukutania, kwa ajili ya huduma yake
yote na kwa ajili ya mavazi matakatifu.
22 Wote waliokuwa na utayari, wanaume
kwa wanawake, wakaja wakaleta vito vya
dhahabu vya kila aina: vipini, vipuli, pete
na mapambo. Wote wakatoa dhahabu zao
kama sadaka ya kuinuliwa kwa BWANA.
23 [e]Kila mmoja aliyekuwa na nyuzi za
rangi ya buluu, za zambarau, au za rangi
nyekundu au kitani safi, au singa za mbuzi,
ngozi za kondoo dume zilizotiwa rangi
nyekundu, au ngozi za pomboo, wakavileta.
24 Wale waliotoa sadaka ya fedha au shaba
wakavileta kama sadaka kwa BWANA, na
kila aliyekuwa na mti wa mshita kwa ajili ya
kazi yoyote ile akauleta. 25 [f]Kila mwanamke
aliyekuwa na ujuzi alisokota kwa mikono
yake na alileta kile alichosokota, iwe ni
nyuzi za rangi ya buluu, za zambarau, au za
rangi nyekundu au kitani safi. 26 [g]Wanawake
wote waliopenda na waliokuwa na ujuzi
wakasokota singa za mbuzi. 27 Viongozi
wakaleta vito vya shohamu pamoja na vito
vingine vya thamani kwa ajili ya kuweka
kwenye kisibau na kwenye kifuko cha
kifuani. 28 [h]Wakaleta pia vikolezi na mafuta
ya zeituni kwa ajili ya mwanga, kwa ajili
ya mafuta ya upako na kwa ajili ya uvumba
wenye harufu nzuri. 29 [i]Waisraeli wote
waume kwa wake waliokuwa wanapenda
wakaleta mbele za BWANA kwa hiari yao
wenyewe sadaka kwa ajili ya kazi yote ya
BWANA aliyokuwa amewaagiza kuifanya
kupitia kwa Mose.

*Bezaleli Na Oholiabu*

**(Kutoka 31:1-11)**

30 Kisha Mose akawaambia Waisraeli,
"Tazameni, BWANA amemchagua Bezaleli
mwana wa Uri, mwana wa Huri, wa
kabila la Yuda, 31 [j]naye amemjaza Roho
wa Mungu, pamoja na ustadi, na uwezo
na ujuzi katika aina zote za ufundi, 32 ili
kubuni michoro ya kupendeza katika ufundi
wa dhahabu, fedha na shaba, 33 kuchonga
vito na kuvitia mahali, kufanya ufundi kwa
mbao, na kujishughulisha na aina zote za
ufundi wa kupendeza. 34 [k]Tena amempa
yeye pamoja na Oholiabu, mwana wa
Ahisamaki, wa kabila la Dani, uwezo wa
kufundisha wengine. 35 [l]Amewajaza ustadi
wa kufanya kazi za aina zote zifanywazo
na mafundi, na wenye kubuni michoro, pia
na watarizi kwa rangi za buluu, zambarau,
nyekundu na kitani safi, na wafumaji: wote
wakiwa mafundi na wabunifu hodari.

36 [m]Kwa hiyo Bezaleli, Oholiabu na kila
mtu BWANA aliyempa ustadi na uwezo wa
kujua jinsi ya kufanya kazi zote za kujenga
mahali patakatifu wataifanya hiyo kazi
kama vile BWANA alivyoagiza."

2 [n]Ndipo Mose akawaita Bezaleli na
Oholiabu na kila mtu mwenye ustadi
ambaye BWANA alikuwa amempa uwezo

[a]**35:17** Kut 27:9; 38:9-20
[b]**35:18** Kut 27:19; 38:20
[c]**35:19** Kut 28:2; 31:10; 39:1
[d]**35:21** Kut 25:2; 36:2; 1Nya 28:2, 9; 29:9; Ezr 7:27; 2Kor 8:12; 9:7
[e]**35:23** Kut 39:1; 1Nya 29:8
[f]**35:25** Kut 28:3; 31:6; 36:1; 2Fal 23:7; Mit 31:19-24
[g]**35:26** Kut 25:2; 1Nya 29:6-8
[h]**35:28** Kut 25:6
[i]**35:29** Kut 25:2-7; 36:3; 2Fal 12:4
[j]**35:31** 2Nya 2:7, 14
[k]**35:34** Kut 31:6; 2Nya 2:14
[l]**35:35** Kut 31:3, 6; 36:1, 2; 1Fal 7:14; 1Nya 2:14; Isa 28:26; Yak 1:5
[m]**36:1** Kut 28:3; 25:8; Ay 32:8; Isa 28:26; Mit 2:6; Kut 25:8; Law 4:6; 19:30; Hes 18:5; 30:8; 1Fal 6:16; Za 96:6; 134:2; Isa 63:18; Eze 5:11; Dan 8:13, 14; Ebr 9:1, 2
[n]**36:2** Kut 31:2, 6; 25:2; 35:2, 26; 1Nya 29:5

na mwenye kupenda kuja na kufanya kazi.
3 [a]Wakapokea kutoka kwa Mose sadaka
zote ambazo Waisraeli walikuwa wameleta
ili kuifanya kazi ya ujenzi wa Mahali
Patakatifu. Nao watu wakaendelea kuleta
sadaka za hiari kila asubuhi. 4 Ikafika wakati
mafundi wote wenye ujuzi waliokuwa
wakiifanya kazi yote ya mahali patakatifu
wakasimamisha kazi zao, 5 [b]wakaja na
kumwambia Mose, "Watu wanaleta vitu
vingi kuliko tunavyohitaji kwa ajili ya kazi
hii ambayo BWANA ameagiza ifanyike."

6 Ndipo Mose akatoa agizo, nao
wakapeleka neno hili katika kambi yote:
"Mtu yeyote mwanaume au mwanamke
asilete tena kitu chochote kwa ajili ya
sadaka ya mahali patakatifu." Hivyo watu
wakazuiliwa kuleta zaidi, 7 [c]kwa sababu
walivyokuwa navyo tayari vilitosha na
kuzidi kuifanya kazi yote.

*Maskani Ya Mungu*

**(Kutoka 26:1-37)**

8 [d]Watu wote wenye ustadi miongoni
mwa wafanyakazi wote wakatengeneza
maskani kwa mapazia kumi ya kitani
iliyosokotwa vizuri, na nyuzi za rangi ya
buluu, za zambarau, na za rangi nyekundu,
naye fundi stadi akatirizi makerubi kwenye
mapazia hayo. 9 Mapazia yote yalitoshana
kwa ukubwa: kila moja lilikuwa na urefu
wa dhiraa ishirini na nane,[e] na upana wa
dhiraa nne[f] 10 Wakayaunganisha mapazia
matano pamoja, pia wakafanya vivyo
hivyo kwa hayo mengine matano. 11 Kisha
wakatengeneza vitanzi vya kitambaa cha
buluu kwenye upindo wa pazia la mwisho
la fungu la kwanza, pia wakafanya vivyo
hivyo na pazia la fungu la mwisho.
12 [g]Wakatengeneza pia vitanzi hamsini katika
pazia mmoja, na vitanzi vingine hamsini
kwenye pazia la mwisho la fungu hilo
lingine, nazo vitanzi vyote vikaelekeana.
13 Kisha wakatengeneza vifungo hamsini
vya dhahabu, na wakavitumia kufunga na
kuunganisha zile fungu mbili za mapazia
pamoja ili maskani ipate kuwa kitu kimoja.

14 [h]Wakatengeneza mapazia kumi na moja
ya singa za mbuzi kwa ajili ya kufunika
maskani. 15 Mapazia hayo kumi na moja
yalikuwa na kipimo kimoja, yaani urefu
wa dhiraa thelathini,[i] na upana wa dhiraa
nne. 16 Wakaunganisha mapazia matano
kuwa fungu moja, na hayo mengine sita
kuwa fungu lingine. 17 Kisha wakatengeneza
vitanzi hamsini kwenye upindo wa pazia
la mwisho la fungu moja, na vivyo hivyo
kwenye upindo wa pazia la mwisho la fungu
hilo lingine. 18 Wakatengeneza vifungo
hamsini vya shaba ili kukaza hema pamoja
kuwa kitu kimoja. 19 [j]Kisha wakatengeneza
kifuniko cha hema kwa ngozi za kondoo
dume zilizotiwa rangi nyekundu, na juu
yake kifuniko cha ngozi za pomboo.[k]

20 [l]Wakatengeneza mihimili ya
kusimamisha ya mti wa mshita kwa ajili
ya maskani. 21 Kila mhimili ulikuwa na
urefu wa dhiraa kumi,[m] na upana wa
dhiraa moja na nusu,[n] 22 zikiwa na ndimi
mbili zilizokuwa sambamba kila mmoja na
mwingine. Wakatengeneza mihimili yote
ya maskani jinsi hii. 23 Wakatengeneza
mihimili ishirini kwa ajili ya upande wa
kusini wa maskani, 24 na wakatengeneza
vitako arobaini vya fedha vya kuweka
chini ya hiyo mihimili, vitako viwili kwa
kila mhimili, kimoja chini ya kila ulimi.
25 Kwa upande wa kaskazini wa maskani
wakatengeneza mihimili ishirini 26 na
vitako arobaini vya fedha, viwili chini ya

[a]**36:3** Kut 35:29
[b]**36:5** 2Nya 24:14; 31:10; 2Kor 8:2-3
[c]**36:7** 1Fal 7:47
[d]**36:8** Kut 26:1; Ay 32:8; Mit 10:8; 15:14; 21:1; Mwa 3:24; 1Fal 6:23; 2Nya 3:10; Eze 1:5-28; 10:1
[e]9 Dhiraa 28 ni sawa na mita 12.6.
[f]9 Dhiraa nne ni sawa na mita 1.8.
[g]**36:12** Kut 26:5
[h]**36:14** Kut 26:7
[i]15 Dhiraa 30 ni sawa na mita 13.5.
[j]**36:19** Kut 26:14
[k]19 *Pomboo* hapa ina maana ya mnyama mwenye ngozi laini aishiye kwenye milima yenye misitu, au pengine nguva au sili.
[l]**36:20** Kut 26:15; 25:5, 10; Hes 25:1; Kum 10:3; Yos 2:1
[m]21 Dhiraa 10 ni sawa na mita 4.5.
[n]21 Dhiraa moja na nusu ni sawa na sentimita 67.5.

kila mhimili. 27 Wakatengeneza mihimili
sita kwa mwisho ulio mbali, yaani upande
wa magharibi wa maskani, 28 na mihimili
miwili ikatengenezwa kwa ajili ya pembe
za maskani za upande uliokuwa mbali.
29 [a]Katika pembe hizi mbili mihimili yake
ilikuwa miwili kuanzia chini mpaka juu,
na ikaingizwa kwenye pete moja; mihimili
ya pembe hizi mbili ilifanana. 30 Kwa hiyo
kulikuwa na mihimili minane, na vitako
kumi na sita vya fedha, viwili chini ya kila
mhimili.

31 [b]Wakatengeneza pia mataruma kwa
mti wa mshita: matano kwa ajili ya
mihimili ya upande mmoja wa maskani,
32 matano kwa ajili ya mihimili ya upande
mwingine, na matano kwa ajili mihimili
ya upande wa magharibi, mwisho kabisa
mwa maskani. 33 Wakatengeneza taruma
la katikati, likapenya katikati ya mihimili
kutoka mwisho mmoja hadi mwisho
mwingine. 34 Wakaifunika hiyo mihimili
kwa dhahabu, na wakatengeneza pete za
dhahabu za kushikilia hayo mataruma.
Pia wakayafunika hayo mataruma kwa
dhahabu.

35 [c]Wakatengeneza pazia la nyuzi za
rangi ya buluu, za zambarau, na za rangi
nyekundu na kitani safi iliyosokotwa
vizuri, naye fundi stadi akatirizi makerubi
kwenye hilo pazia. 36 Wakatengeneza nguzo
nne za mti wa mshita kwa ajili yake na
kuzifunika kwa dhahabu. Wakatengeneza
kulabu za dhahabu kwa ajili ya nguzo hizo,
na kusubu vitako vinne vya fedha. 37 [d]Kwa
ajili ya ingilio la hema wakatengeneza
pazia la nyuzi za rangi ya buluu, za
zambarau, na za rangi nyekundu na kitani
safi iliyosokotwa vizuri, kazi ya mtarizi.
38 [e]Pia wakatengeneza nguzo tano zenye
kulabu. Wakafunika ncha za juu za hizo
nguzo pamoja na tepe zake kwa dhahabu,
na pia wakatengeneza vitako vyake vitano
vya shaba.

*Sanduku La Agano*

**(Kutoka 25:10-22)**

37 [f]Bezaleli akatengeneza Sanduku la
mbao za mshita: urefu wake ulikuwa
dhiraa mbili na nusu,[g] upana wake dhiraa
moja na nusu, na kimo chake dhiraa moja
na nusu. 2 Akalifunika kwa dhahabu safi
ndani na nje, na kulizungushia ukingo wa
dhahabu. 3 Akasubu pete nne za dhahabu na
kuzifungia kwenye miguu yake minne, pete
mbili kwa upande mmoja na pete mbili kwa
upande mwingine. 4 [h]Kisha akatengeneza
mipiko ya mti wa mshita na kuzifunika kwa
dhahabu. 5 [i]Akaiingiza hiyo mipiko kwenye
zile pete katika pande mbili za Sanduku ili
kulibeba.

6 [j]Akatengeneza kifuniko cha upatanisho
kwa dhahabu safi: urefu wake ulikuwa dhiraa
mbili na nusu, na upana wake dhiraa moja
na nusu. 7 [k]Kisha akatengeneza makerubi
wawili wa dhahabu iliyofuliwa katika
miisho ya hicho kifuniko. 8 Akatengeneza
kerubi mmoja kwenye mwisho mmoja,
na kerubi mwingine kwenye mwisho
mwingine; akawatengeneza kuwa kitu
kimoja na hicho kifuniko katika miisho
hiyo miwili. 9 [l]Makerubi hao walikuwa
wametandaza mabawa kuelekea juu,
wakitia kivuli hicho kifuniko. Makerubi hao
walielekeana, wakitazama hicho kifuniko.

*Meza*

**(Kutoka 25:23-30)**

10 [m]Akatengeneza meza ya mbao za

---

[a]**36:29** Kut 26:24; Za 133:1; Mdo 2:46; 1Kor 1:10

[b]**36:31** Kut 26:26

[c]**36:35** Kut 39:38; Mt 27:51; Lk 23:45; Ebr 9:5; 6:19; 10:20

[d]**36:37** Kut 27:16; Law 16:2

[e]**36:38** 1Fal 7:16; 2Nya 4:12; Yer 52:22

[f]**37:1** Kut 31:2; 30:6; 39:35; Kum 10:3; Kut 35:30; 25:10

[g]1 Dhiraa moja na nusu ni sawa na mita 1.13.

[h]**37:4** Hes 4:6

[i]**37:5** Hes 1:50; 2Sam 6:3

[j]**37:6** Kut 26:34; 31:7; Ebr 9:5; Kut 25:17

[k]**37:7** Eze 41:18

[l]**37:9** Ebr 9:5; Kum 10:3; Mwa 3:24; Kut 25:22; 1Fal 6:23; 2Nya 3:10; Za 80:1; Eze 1:5-28; 10:1; Yn 1:51; Flp 2:10; 1Tim 3:16; 1Pet 1:12

[m]**37:10** Kum 31:8; Ebr 9:2; Kut 15:23; Mal 1:7, 12

mshita yenye urefu wa dhiraa mbili,[a] upana
wa dhiraa moja,[b] na kimo cha dhiraa moja
na nusu. 11 Kisha akaifunika kwa dhahabu
safi, na kuitengenezea ukingo wa dhahabu
kuizunguka pande zote. 12 Pia akatengeneza
upapi wenye upana wa nyanda nne,[c] na
kuufanyia ule upapi ukingo wa dhahabu
kuuzunguka pande zote. 13 Akasubu pete
nne za dhahabu kwa ajili ya meza hiyo, na
kuzifungia kwenye pembe nne, pale penye
miguu yake minne. 14 [d]Pete hizo ziliwekwa
karibu na ukingo ule ili kuishikilia ile mipiko
iliyotumika kuibebea hiyo meza. 15 Mipiko
hiyo ya kubebea meza ilitengenezwa kwa
mti wa mshita, na ilikuwa imefunikwa kwa
dhahabu. 16 [e]Vyombo vyote vya mezani
vilitengenezwa kwa dhahabu safi: yaani
sahani zake, masinia, na bakuli na bilauri
zake kwa ajili ya kumiminia sadaka za
vinywaji.

*Kinara Cha Taa*

**(Kutoka 25:31-40)**

17 [f]Akatengeneza kinara cha taa cha
dhahabu safi iliyofuliwa vizuri katika
kitako chake na ufito wake; vikombe
vyake vilivyofanana na ua, matovu na
maua vilikuwa kitu kimoja. 18 Matawi sita
yalitokeza kuanzia ule ufito wa katikati
wa kinara cha taa: matawi matatu upande
mmoja na matatu upande mwingine.
19 Vikombe vitatu vya mfano wa maua ya
mlozi yenye matovu na maua vilikuwa
katika tawi moja, vikombe vitatu katika
tawi jingine, na vivyo hivyo kwa matawi
yote sita yaliyotokeza kwenye kile kinara
cha taa. 20 [g]Juu ya kinara chenyewe
kulikuwepo na vikombe vinne vya mfano
wa maua ya mlozi yakiwa na matovu yake
na maua yake. 21 Tovu moja lilikuwa chini
ya jozi ya kwanza ya matawi yaliyotokeza
kwenye kinara cha taa, tovu la pili chini
ya jozi ya pili, nalo tovu la tatu chini ya
jozi ya tatu, yaani, matawi sita kwa jumla.
22 [h]Matovu na matawi yote yalikuwa kitu
kimoja na kile kinara cha taa, yakiwa
yamefuliwa kwa dhahabu safi.
23 [i]Akatengeneza taa zake saba, na pia
mikasi ya kusawazishia tambi, pamoja
na masinia, zote kwa dhahabu safi.
24 Akatengeneza kinara hicho cha taa
pamoja na vifaa vyake vyote kutumia
talanta[j] moja ya dhahabu safi.

*Madhabahu Ya Kufukizia Uvumba*

**(Kutoka 30:1-5)**

25 [k]Akatengeneza madhabahu ya
kufukizia uvumba kwa mbao za mshita.
Ilikuwa ya mraba, urefu na upana wake
dhiraa moja, na kimo cha dhiraa mbili, nazo
pembe zake zilikuwa kitu kimoja nayo.
26 Akafunika hayo madhabahu juu na pande
zote na pia zile pembe zake kwa dhahabu
safi, na akayafanyizia ukingo wa dhahabu
kuizunguka. 27 Akatengeneza pete mbili
za dhahabu kwa ajili ya madhabahu chini
ya huo ukingo, zikiwa mbili kila upande,
za kushikilia hiyo mipiko iliyotumika
kuyabebea madhabahu. 28 [l]Akatengeneza
mipiko kwa miti ya mshita na kuifunika
kwa dhahabu.
29 [m]Pia akatengeneza mafuta matakatifu
ya upako, na uvumba safi wenye harufu
nzuri, kazi ya mtengeneza manukato.

---

[a]10 Dhiraa mbili ni sawa na sentimita 90.
[b]10 Dhiraa moja ni sawa na sentimita 45.
[c]12 Nyanda nne ni sawa na sentimita 8.
[d]**37:14** Ebr 9:4
[e]**37:16** Kut 25:29
[f]**37:17** Ebr 9:2; Ufu 1:12; Kut 25:31; Law 24:4; 1Nya 28:15; Zek 4:2; Mt 5:15, 16; Yn 5:35; Flp 2:15; 1Pet 2:9; Ufu 1:20
[g]**37:20** Hes 17:8; Yer 1:11
[h]**37:22** Hes 8:4
[i]**37:23** Kut 40:4, 25; Ufu 1:20; 4:5
[j]24 Talanta moja ya dhahabu ni sawa na kilo 34.
[k]**37:25** Kut 30:34-36; Lk 1:11; Ebr 9:4; Ufu 8:3; Kut 27:2; Ufu 9:13; 1Fal 9:25; 1Nya 29:6, 7; Isa 60:6; Mal 1:11; 1Pet 2:5
[l]**37:28** Kut 25:13
[m]**37:29** Kut 31:11; 30:1, 25; 39:38; Isa 61:1; 11:2; Za 133:2; 1Yn 2:20; Za 141:2; Wim 4:14; Mal 1:11; Ebr 5:7; 7:25; Ufu 5:8; 8:3, 4

*Madhabahu Ya Sadaka Ya Kuteketezwa*

**(Kutoka 27:1-8)**

38 [a]Akatengeneza madhabahu ya sadaka
ya kuteketezwa kwa mbao za mti wa
mshita, kimo chake dhiraa tatu;[b] nayo
ilikuwa mraba, urefu wake dhiraa tano,
na upana wa dhiraa tano[c] 2 [d]Akatengeneza
upembe kwenye kila pembe ya hizo pembe
nne, ili zile pembe na madhabahu zikawa
zimeungana, akafunika madhabahu kwa
shaba. 3 [e]Akatengeneza vyombo vyake
vyote kwa shaba: vyungu vyake vya
kuondolea majivu, masepetu, mabakuli ya
kunyunyizia, uma za nyama na vyombo
vya kuchukulia moto. 4 Akatengeneza wavu
wa shaba chini ya ukingo wa madhabahu
ili ufikie nusu ya kimo cha madhabahu.
5 Akasubu pete za shaba za kushikilia ile
mipiko kwa ajili ya zile pembe nne za huo
wavu wa shaba. 6 Akatengeneza mipiko
ya mti wa mshita na kuifunika kwa shaba.
7 Akaiingiza ile mipiko kwenye zile pete, ili
iwe pande mbili za madhabahu kwa ajili ya
kuibeba. Akaitengeneza madhabahu yenye
uvungu ndani yake akitumia mbao.

*Sinia La Kunawia*

**(Kutoka 30:18)**

8 [f]Akatengeneza sinia la shaba lenye
kitako cha shaba kutoka kwa vioo vya shaba
vilivyotolewa na wanawake waliohudumu
pale ingilio la Hema la Kukutania.

*Ua Wa Hema La Kukutania*

**(Kutoka 27:9-19)**

9 [g]Kisha akatengeneza ua. Upande wa
kusini ulikuwa na urefu wa dhiraa mia
moja,[h] na ulikuwa na mapazia ya kitani
iliyosokotwa vizuri, 10 pamoja na nguzo
ishirini na vitako vya shaba ishirini, na
kulabu na tepe za fedha juu ya hizo nguzo.
11 Upande wa kaskazini ulikuwa na urefu
wa dhiraa mia moja, pamoja na nguzo
ishirini na vitako vya shaba ishirini, pamoja
na kulabu na tepe za fedha juu ya hizo
nguzo.

12 Upande wa mwisho wa magharibi
ulikuwa na upana wa dhiraa hamsini[i] na
ulikuwa na mapazia, na nguzo kumi na
vitako vyake kumi, pamoja na kulabu
na tepe za fedha juu ya hizo nguzo.
13 Upande wa mwisho wa mashariki jua
linakochomoza, pia ulikuwa na upana wa
dhiraa hamsini. 14 Mapazia yenye urefu
wa dhiraa kumi na tano[j] yalikuwa upande
mmoja wa ingilio, pamoja na nguzo tatu
na vitako vitatu. 15 Mapazia yenye urefu
wa dhiraa kumi na tano yalikuwa upande
mwingine wa ingilio la ua, pamoja na
nguzo tatu na vitako vitatu. 16 Mapazia
yote yaliyozunguka ua yalikuwa ya kitani
iliyosokotwa vizuri. 17 Vitako vya nguzo
vilikuwa vya shaba. Kulabu na tepe juu
ya nguzo zilikuwa za fedha, na ncha zake
zilifunikwa kwa fedha. Kwa hiyo nguzo zote
za ua zilikuwa na tepe za fedha.

18 [k]Pazia la ingilio la ua lilikuwa la nyuzi
za rangi ya buluu, za zambarau, na za rangi
nyekundu pamoja na kitani iliyosokotwa
vizuri, kazi ya mtarizi. Pazia hilo lilikuwa
na urefu wa dhiraa ishirini kama zile
za kwenye ua, na kimo chake kilikuwa
dhiraa tano, 19 likiwa na nguzo nne na
vitako vinne vya shaba. Kulabu zake na
tepe zake zilikuwa za fedha, na ncha zake
zilikuwa zimefunikwa kwa fedha. 20 [l]Vigingi
vyote vya maskani na vya ua ulioizunguka
vilikuwa vya shaba.

---

[a]**38:1** Kut 27:1; 2Nya 29:23, 24; Za 51:15-19; Isa 61:8; Eze 44:11; 45:17; Ebr 9:14; 13:10
[b]1 Dhiraa 3 ni sawa na mita 1.35.
[c]1 Dhiraa 5 ni sawa na mita 2.25.
[d]**38:2** 2Nya 1:5; 1Fal 7:45
[e]**38:3** Kut 31:9; 35:16
[f]**38:8** Kut 30:18; 40:7; Kum 23:17; 1Sam 2:22; 1Fal 14:24; 2Fal 16:17; 2Nya 4:2; Za 26:6; Zek 13:1; Eze 36:25; 2Kor 7:1; Ebr 10:22; 1Yn 5:6
[g]**38:9** Kut 27:9; Za 84:2; 92:13
[h]9 Dhiraa 100 ni sawa na mita 45.
[i]12 Dhiraa 50 ni sawa na mita 22.5.
[j]14 Dhiraa 15 ni sawa na mita 6.75.
[k]**38:18** 2Nya 3:14
[l]**38:20** Kut 35:18; 38:20; 27:10; 2Nya 3:9; Ezr 9:8; Isa 22:23; Efe 2:21, 22

*Vifaa Vilivyotumika*

21 [a]Ifuatayo ni orodha ya vifaa vilivyotumika kwa ajili ya ujenzi wa maskani, maskani ya Ushuhuda, ambavyo vilitayarishwa na Walawi kama alivyoagiza Mose, chini ya usimamizi wa Ithamari, mwana wa kuhani Aroni. 22 [b](Bezaleli mwana wa Uri, mwana wa Huri, wa kabila la Yuda, alifanya kila kitu BWANA alichomwamuru Mose, 23 [c]akiwa pamoja na Oholiabu mwana wa Ahisamaki, wa kabila la Dani, fundi stadi wa kutia nakshi, kubuni michoro, mtarizi kwa rangi ya buluu, ya zambarau, nyekundu na kitani safi.) 24 [d]Jumla ya dhahabu iliyopatikana kutokana na sadaka ya kuinuliwa kwa ajili ya kazi ya mahali patakatifu ilikuwa na uzito wa talanta 29 na shekeli 730,[e] kulingana na shekeli ya mahali patakatifu.

25 [f]Fedha iliyopatikana kutokana na jumuiya ya watu waliohesabiwa ilikuwa yenye uzito wa talanta mia moja na shekeli 1,775,[g] kulingana na shekeli ya mahali patakatifu. 26 [h]Kila mtu alitoa beka moja, ambayo ni sawa na nusu shekeli ya fedha, kwa kazi ya mahali patakatifu, kutoka kwa kila mtu aliyekuwa amehesabiwa mwenye umri wa miaka ishirini au zaidi, ambao jumla yao walikuwa wanaume 603,550.
27 [i]Talanta hizo 100 za fedha zilitumika kusubu vile vitako mia moja kwa ajili ya mahali patakatifu na pazia: vitako mia moja kwa talanta mia, yaani, talanta moja kwa kila kitako. 28 Akatumia zile shekeli hizo 1,775 kutengeneza kulabu za nguzo, kufunika ncha za nguzo na kutengeneza vitanzi vyake.

29 Shaba iliyopatikana kutokana na sadaka ya kuinuliwa ilikuwa na uzito wa talanta 70 na shekeli 2,400.[j] 30 Akaitumia hiyo shaba kutengeneza vitako vya ingilio la Hema la Kukutania, madhabahu ya shaba pamoja na ule wavu wake na vyombo vyake vyote, 31 [k]vile vitako vya ule ua uliozunguka na vile vya ingilio, na vigingi vyote vya Maskani pamoja na ule ua uliozunguka.

*Mavazi Ya Kikuhani*

**(Kutoka 28:1-14)**

39 [l]Kutokana na nyuzi za rangi ya buluu, ya zambarau na nyekundu akatengeneza mavazi yaliyofumwa kwa ajili ya kuhudumu katika mahali patakatifu. Pia akamshonea Aroni mavazi matakatifu, kama BWANA alivyomwagiza Mose.

*Kisibau*

2 [m]Akatengeneza kisibau cha dhahabu, na nyuzi za rangi ya buluu, za zambarau, na nyekundu na kitani iliyosokotwa vizuri. 3 Akafua vipande vyembamba vya dhahabu kwa nyundo na kutengeneza nyuzi nyembamba ili kuzifuma pamoja na hizo nyuzi za rangi ya buluu, za zambarau, na za rangi nyekundu na kitani safi, kazi ya fundi stadi. 4 [n]Akatengeneza vipande vya mabegani vya kisibau, vilivyoshikizwa kwenye pembe zake mbili ili kukifungia kisibau. 5 [o]Mshipi wa kiunoni uliofumwa kwa ustadi ulifanana nacho: ulikuwa kitu kimoja na hicho kisibau, nao ulitengenezwa kwa dhahabu na nyuzi za rangi ya buluu, za zambarau, na nyekundu na kwa kitani iliyosokotwa vizuri, kama BWANA alivyomwagiza Mose.

6 [p]Akatengeneza vito vya shohamu vilivyowekwa katika vijalizo vya dhahabu, navyo vilichorwa na majina ya wana wa

[a]**38:21** Hes 1:50-53; 8:24; 9:15; 10:11; 17:7; 1Nya 23:32; 2Nya 24:6; Mdo 7:44; Ufu 15:5; Hes 4:28-33
[b]**38:22** Kut 31:2
[c]**38:23** Kut 31:6
[d]**38:24** Kut 30:12-16; 12:37; Hes 3:47
[e]24 Talanta 29 na shekeli 730 ni sawa na tani moja.
[f]**38:25** Kut 12:37; 30:12
[g]25 Talanta 100 na shekeli 1,775 za fedha ni sawa na tani 3.4.
[h]**38:26** Kut 30:12-16; 12:36-37; Hes 1:46
[i]**38:27** Kut 26:19
[j]29 Talanta 70 na shekeli 2,400 ni sawa na tani 2.4.
[k]**38:31** Kut 27:19; 2Nya 3:9; Ezr 9:8; Isa 22:23; Efe 2:21, 22
[l]**39:1** Kut 35:19-23; 28:2; Za 93:5; Eze 43
[m]**39:2** Kut 28:6; Law 8:7
[n]**39:4** Law 24:7; Yos 4:7
[o]**39:5** Isa 11:5; Ufu 1:13
[p]**39:6** Kut 28:9; Ay 28:16; Isa 49:16; Ufu 1:17

Israeli kama vile muhuri huchorwa. 7 [a]Kisha
akavifungia kwenye vipande vya mabega ya
kisibau kuwa vito vya ukumbusho kwa wana
wa Israeli, kama BWANA alivyomwagiza
Mose.

*Kifuko Cha Kifuani*

**(Kutoka 28:15-30)**

8 [b]Akafanyiza kifuko cha kifuani, kazi
ya fundi stadi. Akakitengeneza kama kile
kisibau: cha dhahabu, na nyuzi za rangi ya
buluu, za zambarau, na za rangi nyekundu,
cha kitani safi iliyosokotwa. 9 Kifuko hicho
kilikuwa cha mraba, chenye urefu wa
shibiri moja[c] na upana wa shibiri moja,
nacho kilikunjwa mara mbili. 10 [d]Kifuko
hicho kilipambwa kwa safu nne za vito
vya thamani. Safu ya kwanza ilikuwa na
akiki, yakuti manjano na zabarajadi; 11 [e]safu
ya pili ilikuwa na almasi, yakuti samawi
na zumaridi; 12 safu ya tatu ilikuwa na
hiakintho, akiki nyekundu na amethisto;
13 [f]katika safu ya nne ilikuwa na krisolitho,
shohamu na yaspi. Vito hivyo vilitiwa
kwenye vijalizo vya dhahabu. 14 [g]Palikuwa
na vito kumi na viwili, kila kimoja kikiwa
na jina mojawapo la wana wa Israeli; kila
kimoja kilichorwa kama muhuri kikiwa na
jina mojawapo la yale makabila kumi na
mawili.

15 Kwa ajili ya kile kifuko cha kifuani
akakitengenezea mikufu ya dhahabu safi,
iliyosokotwa kama kamba. 16 Akatengeneza
vijalizo viwili vya dhahabu na pete mbili
za dhahabu, na kuzifungia pete hizo
kwenye pembe mbili za hicho kifuko cha
kifuani. 17 Akafunga hiyo mikufu miwili ya
dhahabu kwenye hizo pete katika pembe za
hicho kifuko cha kifuani, 18 nazo zile ncha
nyingine za mkufu akazifunga kwenye vile
vijalizo viwili, na kuzishikamanisha na vile
vipande vya mabega vya kile kisibau upande
wa mbele. 19 Akatengeneza pete mbili za
dhahabu na kuzishikamanisha kwenye
pembe mbili za chini, upande wa ndani
wa kifuko cha kifuani karibu na kisibau.
20 Kisha akatengeneza pete nyingine mbili
za dhahabu na kuzishikamanisha sehemu
ya chini ya vipande vya mabega upande wa
mbele wa kile kisibau, karibu na pindo juu
kidogo ya mshipi wa kiunoni wa kisibau.
21 Akafunga pete za hicho kifuko cha kifuani
kwenye pete za kisibau kwa kamba ya
buluu, wakiziunganisha na ule mshipi wa
kiunoni, ili kifuko cha kifuani kisisogee
kutoka kwenye kile kisibau, kama BWANA
alivyomwagiza Mose.

*Mavazi Mengine Ya Kikuhani*

**(Kutoka 28:31-43)**

22 [h]Akashona joho la kisibau lote kwa
kitambaa cha rangi ya buluu tupu, kazi ya
mfumaji, 23 na lilikuwa na nafasi ya shingo
katikati ya joho lile iliyofanana na ukosi, na
utepe ulioshonwa kuizunguka nafasi hiyo ili
isichanike. 24 Akatengeneza makomamanga
ya nyuzi za rangi ya buluu, za zambarau, na
nyekundu na ya kitani iliyosokotwa vizuri
kuzunguka pindo la hilo joho. 25 [i]Kisha
akatengeneza vikengele vya dhahabu safi
na kuvishikamanisha kuzunguka pindo
hilo kati ya hayo makomamanga. 26 Hivyo
vikengele na makomamanga vilipishana
kuzunguka upindo wa joho ili livaliwe kwa
kuhudumu, kama BWANA alivyomwagiza
Mose.

27 [j]Pia akamtengenezea Aroni na wanawe
makoti ya kitani safi, kazi ya mfumaji, 28 [k]na
kilemba cha kitani safi, tepe za kichwani
za kitani, na nguo za ndani za kitani
iliyosokotwa vizuri. 29 Mshipi ulikuwa wa
kitani iliyosokotwa vizuri ya rangi ya buluu,
na zambarau, na nyekundu, kazi ya mtarizi,
kama BWANA alivyomwagiza Mose.

---

[a]**39:7** Law 24:7; Yos 4:7; Kut 28:12; Yos 4:7; Neh 2:20
[b]**39:8** Law 8:8; Kut 28:15; Isa 59:17
[c]9 Shibiri moja ni sawa na sentimita 22.
[d]**39:10** Kut 28:17; Eze 28:13; Ufu 21:19, 20; Isa 54:12
[e]**39:11** Ufu 4:3; Isa 54:11; Yer 17:1
[f]**39:13** Dan 10:6; Ay 28:16; Ufu 21:11
[g]**39:14** Ufu 21:12
[h]**39:22** Kut 28:31; Law 8:7; 1Sam 2:18; 2Sam 6:14
[i]**39:25** Kut 28:33
[j]**39:27** Kut 28:39, 40; 39:27; Law 8:13; Kut 28:4; Isa 61:10; Rum 3:22; Gal 3:27
[k]**39:28** Law 6:10; 8:2; Kut 28:39, 42; Eze 44:17, 18

30 [a]Kisha akatengeneza lile bamba, taji
takatifu, kwa dhahabu safi na kuchora
juu yake maneno haya kama vile muhuri
huchorwa: Mtakatifu kwa Bwana.
31 Kisha wakalifunga kwa kamba ya rangi ya
buluu ili kulishikamanisha na kile kilemba
kama Bwana alivyomwagiza Mose.

### *Mose Akagua Maskani Ya Mungu*

**(Kutoka 35:10-19)**

32 [b]Kwa hiyo kazi yote ya maskani,
Hema la Kukutania ikakamilika. Waisraeli
wakafanya kila kitu sawasawa kama vile
Bwana alivyomwagiza Mose. 33 [c]Ndipo
wakaleta maskani kwa Mose: hema
pamoja na vifaa vyake vyote, vibanio
vyake, mihimili yake, mataruma yake,
nguzo na vitako vyake; 34 kifuniko cha
ngozi za kondoo dume kilichotiwa rangi
nyekundu, kifuniko cha ngozi za pomboo,[d]
pazia la kufunikia; 35 [e]Sanduku la Ushuhuda
pamoja na mipiko yake na kiti cha rehema,
36 [f]meza pamoja na vyombo vyake vyote
na mikate ya Wonyesho; 37 [g]kinara cha
taa cha dhahabu safi, safu zake za taa
pamoja na vifaa vyake vyote pamoja na
mafuta kwa ajili ya taa; 38 [h]madhabahu ya
dhahabu, mafuta ya upako, uvumba wenye
harufu nzuri na pazia la ingilio la hema;
39 [i]madhabahu ya shaba, pamoja na wavu
wa shaba, nguzo zake na vyombo vyake
vyote, sinia, na tako lake; 40 [j]mapazia ya
ua pamoja na nguzo na vitako vyake, pia
na pazia kwa ajili ya ingilio la kwenye ua;
kamba zake na vigingi vya hema kwa ajili
ya ua; vyombo vyote vilivyohitajiwa kwa
ajili ya maskani, Hema la Kukutania; 41 na
mavazi yaliyofumwa yanayovaliwa wakati
wa huduma katika mahali patakatifu, yaani
mavazi matakatifu ya kuhani Aroni na
mavazi kwa ajili ya wanawe watakapokuwa
wakihudumu katika kazi ya ukuhani.
42 [k]Waisraeli walikuwa wamefanya kazi
yote sawasawa na vile Bwana alivyokuwa
amemwagiza Mose. 43 [l]Mose akakagua kazi
na kuona kuwa walikuwa wameifanya
sawasawa kama vile Bwana alivyokuwa
ameagiza. Kwa hiyo Mose akawabariki.

### *Kuweka Wakfu Maskani Ya Mungu*

40 Kisha Bwana akamwambia Mose:
2 [m]"Simika Maskani ya Mungu, yaani
Hema la Kukutania, katika siku ya kwanza
ya mwezi wa kwanza. 3 [n]Weka Sanduku
la Ushuhuda ndani yake na ulifunike
kwa pazia. Ingiza meza na kupanga vitu
vyake juu yake. 4 [o]Kisha ingiza kinara cha
taa na uweke taa zake juu yake. 5 [p]Weka
madhabahu ya dhahabu ya kufukizia
uvumba mbele ya Sanduku la Ushuhuda
kisha uweke pazia kwenye lango la Maskani
ya Mungu.
6 [q]"Weka madhabahu ya sadaka za
kuteketezwa mbele ya lango la Maskani
ya Mungu, yaani Hema la Kukutania;
7 [r]weka sinia kati ya Hema la Kukutania
na madhabahu, na uweke maji ndani yake.
8 [s]Fanyiza ua kuzunguka maskani na uweke
pazia penye ingilio la ua.
9 [t]"Chukua mafuta ya upako, ipake
Maskani ya Mungu pamoja na kila kitu
kilichomo ndani yake; iweke wakfu pamoja
na vitu vyote vilivyomo ndani mwake, nayo

---

[a]**39:30** Isa 23:18; Zek 14:20; Za 93:5; Isa 23:18
[b]**39:32** Kut 25:9; 25:40
[c]**39:33** Kut 25:8-40; 36:10-16; Ebr 9:1-28
[d]34 *Pomboo* hapa ina maana ya mnyama mwenye ngozi laini aishiye kwenye milima yenye misitu, au pengine nguva au sili.
[e]**39:35** Kut 30:6; 37:1
[f]**39:36** Kut 25:23-30; 37:10-16
[g]**39:37** Kut 25:31-39; 25:6; Ufu 1:13-20; Mt 5:14; Flp 2:15
[h]**39:38** Kut 31:1-10; 37:25-28; 30:22-32; 37:29; 30:34-38; 36:35
[i]**39:39** Kut 37:1-8; 38:1-7; 30:18
[j]**39:40** Kut 27:9-19; 38:9-20; Ufu 3:12
[k]**39:42** Kut 25:9
[l]**39:43** Kut 25:9; 35:10; Mwa 31:55; Law 9:22-23; Hes 6:23-27; Kum 26:15; 2Sam 6:18; 1Fal 8:14, 55; 1Nya 16:2; 2Nya 30:27
[m]**40:2** Kut 26:30; Law 3:2; 6:26; 9:23; 16:16; Hes 7:89; 11:16; 17:4; 20:6; Yos 18:1; 19:51; Yer 7:12; Kut 12:2; Hes 9:1
[n]**40:3** Kut 26; 33; Hes 4:5
[o]**40:4** Kut 25:23; 25:30-31; 26:33
[p]**40:5** Kut 30:1
[q]**40:6** Kut 27:1; 2Fal 16:14; 2Nya 4:1
[r]**40:7** Kut 30:18
[s]**40:8** Kut 27:9
[t]**40:9** Kut 30:26; Hes 7:1; Law 8:10

itakuwa takatifu. 10 [a]Kisha yapake mafuta
hayo madhabahu ya kuteketezea sadaka
pamoja na vifaa vyake vyote; weka wakfu
madhabahu nayo yatakuwa takatifu sana.
11 Paka sinia mafuta pamoja na kishikilio
chake na uviweke wakfu.

12 [b]"Mlete Aroni na wanawe kwenye
ingilio la Hema la Kukutania na uwaoshe
kwa maji. 13 [c]Kisha mvike Aroni yale
mavazi matakatifu, umtie mafuta na
kumweka wakfu ili apate kunitumikia
katikati ya ukuhani. 14 [d]Walete wanawe
na uwavike makoti. 15 [e]Kisha watie mafuta
kama ulivyomtia baba yao, ili nao pia
wanitumikie katika kazi ya ukuhani. Kutiwa
mafuta kwao kutakuwa kwa ajili ya ukuhani
utakaoendelea kwa vizazi vyote vijavyo."
16 [f]Mose akafanya kila kitu sawa kama vile
BWANA alivyomwagiza.

17 [g]Kwa hiyo Maskani ya Mungu
ilisimikwa katika siku ya kwanza ya mwezi
wa kwanza, katika mwaka wa pili. 18 [h]Mose
alipoweka wakfu Maskani ya Mungu,
aliweka vitako mahali pake, akasimamisha
mihimili, akatia mataruma na kusimamisha
nguzo. 19 [i]Kisha akalitandaza hema juu ya
Maskani ya Mungu na kuifunika hema,
kama BWANA alivyomwagiza.

20 [j]Akachukua ule Ushuhuda na kuuweka
ndani ya Sanduku la Agano, akaweka ile
mipiko ya kubebea hilo Sanduku na kuweka
kiti cha rehema juu yake. 21 [k]Kisha Mose
akalileta Sanduku ndani ya Maskani ya
Mungu, akatundika pazia ili kulifunika
Sanduku la Ushuhuda, kama BWANA
alivyomwagiza.

22 [l]Mose akaweka meza ndani ya Hema
la Kukutania, upande wa kaskazini ya
Maskani ya Mungu nje ya pazia 23 [m]na
kupanga mikate juu yake mbele za BWANA,
kama BWANA alivyomwagiza.

24 [n]Akaweka kinara cha taa ndani ya
Hema la Kukutania mkabala na meza
upande wa kusini mwa Maskani ya Mungu
25 [o]na kuziweka taa mbele za BWANA, kama
BWANA alivyomwagiza.

26 [p]Mose akaweka madhabahu ya dhahabu
ndani ya Hema la Kukutania mbele ya pazia
27 [q]na kufukiza uvumba wenye harufu nzuri,
kama BWANA alivyomwagiza. 28 [r]Kisha
akaweka pazia kwenye ingilio la Maskani
ya Mungu.

29 [s]Mose akaweka madhabahu ya sadaka
za kuteketezwa karibu na ingilio la Maskani
ya Mungu, yaani Hema la Kukutania, na
kutoa juu yake sadaka za kuteketezwa
na sadaka za nafaka kama BWANA
alivyomwagiza.

30 [t]Akaweka sinia kati ya Hema la
Kukutania na madhabahu, akaweka maji
ndani yake kwa ajili ya kunawia, 31 [u]Naye
Mose, Aroni na wanawe wakayatumia
kwa kunawia mikono na miguu yao.
32 [v]Wakanawa kila walipoingia katika Hema
la Kukutania au walipoikaribia madhabahu
kama BWANA alivyomwagiza Mose.

33 [w]Kisha Mose akafanya ua kuizunguka
Maskani ya Mungu na madhabahu, pia
akaweka pazia kwenye ingilio la huo ua.
Hivyo Mose akaikamilisha kazi.

### *Utukufu Wa BWANA*

**(Hesabu 9:15-23)**

34 [x]Ndipo wingu likafunika Hema la

[a]**40:10** Kut 29; 36
[b]**40:12** Hes 8:9; Kut 29:4; 30:19
[c]**40:13** Kut 28:41; Law 8:1-12
[d]**40:14** Kut 28:40; Law 10:5
[e]**40:15** Kut 29:9; Hes 25:13
[f]**40:16** Mwa 6:22
[g]**40:17** Hes 7:10
[h]**40:18** 2Nya 1:3; Kut 36:20-34
[i]**40:19** Kut 36:19; Mwa 6:22
[j]**40:20** Kut 16:34; Ebr 9:4; 1Fal 8:9; Kut 25:17-22; 26:34; 31:7
[k]**40:21** Kut 26:33; Mwa 6:22
[l]**40:22** Kut 25:23
[m]**40:23** Kut 25:30; Law 24:5-8; Mwa 6:22
[n]**40:24** Kut 25:31; 26:35
[o]**40:25** Kut 25:37; 37:23; Mwa 6:22
[p]**40:26** Kut 30:1
[q]**40:27** Mwa 6:22; Kut 30:7
[r]**40:28** Kut 26:36
[s]**40:29** Kut 20:24; 29:38-42; Mwa 6:22
[t]**40:30** Kut 30:18
[u]**40:31** Kut 30:19-21
[v]**40:32** Kut 30:20; Mwa 6:22
[w]**40:33** Kut 27:9; 38:9-20; 27:16
[x]**40:34** Kut 19:16; 16:7; Law 16:2; Hes 9:15-23; 1Fal 8:12; 2Nya 5:13; Isa 6:4; Eze 10:4; Kut 19:16; 23; 2Nya 5:13; Yn 1:14; 12:41; Ufu 15:8

Kukutania, na utukufu wa BWANA ukaijaza
Maskani ya Mungu. 35 [a]Mose hakuweza
kuingia ndani ya Hema la Kukutania kwa
sababu wingu lilikuwa limetua juu ya
Hema, nao utukufu wa BWANA ukaijaza
Maskani ya Mungu.
36 [b]Katika safari yote ya Waisraeli, kila
wakati wingu lilipoinuka kutoka juu ya
Maskani ya Mungu, wangeondoka; 37 lakini
kama wingu halikuinuka, hawakuondoka,
mpaka siku lilipoinuka. 38 [c]Kwa hiyo wingu
la BWANA lilikuwa juu ya maskani mchana,
na moto ulikuwa katika hilo wingu wakati
wa usiku, machoni pa nyumba yote ya
Israeli siku zote za safari zao.

---

[a] **40:35** Kut 16:10; 1Fal 8:11; 2Nya 5:13-14; 7:2
[b] **40:36** Hes 9:17-23; 10:13; Neh 9:19
[c] **40:38** Hes 9:15; Kut 13:21; 1Kor 10:1

# MAMBO YA WALAWI

*Sadaka Ya Kuteketezwa*

1 [a]BWANA akamwita Mose na kusema
naye kutoka kwenye Hema la Kukutania,
akamwambia, 2 [b]“Sema na Waisraeli na
uwaambie, ‘Yeyote miongoni mwenu
aletapo sadaka ya mnyama kwa BWANA,
alete mnyama kama sadaka yake kutoka
kundi lake la ng’ombe au la kondoo na
mbuzi.
3 [c]“ ‘Kama sadaka hiyo ni ya kuteketezwa
kutoka kwenye kundi la ng’ombe, atamtoa
ng’ombe dume asiye na dosari. Ni lazima
amlete kwenye ingilio la Hema la Kukutania
ili aweze kukubalika kwa BWANA.
4 [d]Ataweka mkono wake juu ya kichwa cha
sadaka ya kuteketezwa, nayo itakubaliwa
kwa niaba yake ili kufanya upatanisho
kwa ajili yake. 5 [e]Atamchinja yule fahali
mchanga mbele za BWANA, kisha wana
wa Aroni walio makuhani wataleta damu
na kuinyunyiza pande zote za madhabahu
yaliyo penye ingilio la Hema la Kukutania.
6 [f]Ataichuna hiyo sadaka ya kuteketezwa na
kuikata vipande vipande. 7 [g]Wana wa Aroni
kuhani wataweka moto juu ya madhabahu
na kupanga kuni juu ya huo moto. 8 [h]Kisha
wana wa Aroni walio makuhani watapanga
vile vipande vya nyama, pamoja na kichwa
na mafuta ya huyo mnyama juu ya zile kuni
zinazowaka juu ya madhabahu. 9 [i]Ataziosha
sehemu za ndani na miguu yake kwa maji,
naye kuhani atavichoma vyote juu ya
madhabahu. Hii ni sadaka ya kuteketezwa,
sadaka iliyotolewa kwa moto, yenye harufu
nzuri ya kumpendeza BWANA.
10 [j]“ ‘Kama sadaka ni ya kuteketezwa
kutoka kwenye kundi la kondoo au mbuzi,
atamtoa mnyama dume asiye na dosari.
11 [k]Atamchinjia upande wa kaskazini wa
madhabahu mbele za BWANA, nao wana
wa Aroni walio makuhani watanyunyizia
damu yake pande zote za madhabahu.
12 Atamkata vipande vipande, naye kuhani
atavipanga, pamoja na kichwa na mafuta
ya mnyama juu ya zile kuni zinazowaka juu
ya madhabahu. 13 [l]Ataosha sehemu za ndani
na miguu kwa maji, naye kuhani atavileta
vyote na kuvichoma juu ya madhabahu.
Hii ni sadaka ya kuteketezwa, sadaka
iliyotolewa kwa moto, harufu nzuri ya
kumpendeza BWANA.
14 [m]“ ‘Kama sadaka ya kuteketezwa
inayotolewa kwa BWANA ni ndege, atamtoa
hua au kinda la njiwa. 15 [n]Kuhani atamleta
kwenye madhabahu, naye atamvunja shingo
na kumnyofoa kichwa na kumchoma juu
ya madhabahu. Damu yake itachuruzishwa
ubavuni mwa madhabahu. 16 [o]Ataondoa
kifuko cha chakula pamoja na uchafu
wake na kuvitupa upande wa mashariki
wa madhabahu, mahali pale penye majivu.
17 [p]Atampasua na kumweka wazi katika
mabawa yake, lakini asimwachanishe
kabisa, kisha kuhani ataichoma juu ya zile
kuni zinazowaka juu ya madhabahu. Hii ni

---

[a]**1:1** Kut 3:4; 19:3; 25:22; 40:2; Hes 7:89; 12:4-5
[b]**1:2** Law 22:18-21; 7:16, 38; 23:38; 27:9; Hes 15:3
[c]**1:3** Kum 15:21; 12:5-6, 11; Mwa 8:20; Law 6:25; 17:9; 22:19-20, 27; Ezr 8:35; Mal 1:8; Kut 12:5; Ebr 9:14; 1Pet 1:19; Hes 6:16; Isa 58:5
[d]**1:4** Kut 29:10, 15, 36; Law 4:29; 6:25; Eze 45:15; Mwa 32:20, 30; 2Nya 29:23-24; Kut 29:26; 32:30; Isa 56:7; Rum 12:1; Hes 15:25; Flp 4:18; Ebr 10:11
[e]**1:5** Kut 29:11, 20; Law 3:2, 8; 8:2; 10:6; 21:1; Hes 15:8; Kum 13:8; Za 50:9; 69:31; Ebr 12:24; 1Pet 1:2
[f]**1:6** Law 7:8; Kut 29:17
[g]**1:7** Mwa 22:9; Law 3:5; 6:12
[h]**1:8** Kut 29:13; Law 8:20; 9:13
[i]**1:9** Kut 29:17, 18; Law 2:2; 3:5; 17:6; 6:22; 9:14; 23:8, 25, 36; Hes 28:6, 19; 18:17; 28:11-13; Mwa 8:21; Efe 2:5
[j]**1:10** Mwa 22:7; Kut 12:5; Law 3:12; 4:23, 28; 5:6; Hes 15:11
[k]**1:11** Kut 29:11, 20
[l]**1:13** Kut 29:17; Law 6:22; Kum 12:27
[m]**1:14** Mwa 15:9; Lk 2:24; Law 5:7; Lk 2:24
[n]**1:15** Law 5:8-9
[o]**1:16** Law 4:12; 6:10; Hes 4:13
[p]**1:17** Mwa 15:10; Law 5:8

sadaka ya kuteketezwa, sadaka iliyotolewa
kwa moto, harufu nzuri ya kumpendeza
BWANA.

*Sadaka Ya Nafaka*

2 [a]“ ‘Mtu yeyote aletapo sadaka ya nafaka
kwa BWANA, sadaka yake itakuwa ya
unga laini. Atamimina mafuta juu yake,
aweke uvumba juu yake, 2 [b]naye atapeleka
kwa makuhani wana wa Aroni. Kuhani
atachukua konzi moja iliyojaa unga laini
na mafuta pamoja na uvumba wote, na
kuuteketeza kama sehemu ya kumbukumbu
juu ya madhabahu, sadaka iliyotolewa kwa
moto, harufu nzuri ya kumpendeza BWANA.
3 [c]Sadaka ya nafaka iliyobaki ni ya Aroni na
wanawe, ni sehemu ya sadaka iliyo takatifu
sana iliyotolewa kwa BWANA kwa moto.
4 [d]“ ‘Kama utaleta sadaka ya nafaka
iliyookwa jikoni, itakuwa ya unga laini:
maandazi yaliyotengenezwa bila kutiwa
chachu, yaliyochanganywa na mafuta,
au mikate myembamba iliyotengenezwa
bila kutiwa chachu, na iliyopakwa
mafuta. 5 [e]Iwapo sadaka yako ya nafaka
imeandaliwa kwenye kikaango, itakuwa
ni ya unga laini uliochanganywa na mafuta,
bila chachu. 6 Ukande na kumimina mafuta
juu yake; hii ni sadaka ya nafaka. 7 [f]Kama
sadaka yako ya nafaka imepikwa kwenye
sufuria, itatengenezwa kwa unga laini
na mafuta. 8 Ilete hiyo sadaka ya nafaka
iliyotengenezwa kwa vitu hivi kwa BWANA;
mkabidhi kuhani ambaye ataipeleka
madhabahuni. 9 [g]Naye atatoa ile sehemu ya
kumbukumbu kutoka kwenye hiyo sadaka
ya nafaka na kuiteketeza juu ya madhabahu
kuwa sadaka iliyotolewa kwa moto, harufu
nzuri ya kumpendeza BWANA. 10 [h]Sadaka ya
nafaka iliyobaki ni ya Aroni na wanawe;
ni sehemu ya sadaka iliyo takatifu sana ya
sadaka iliyotolewa kwa BWANA kwa moto.
11 [i]“ ‘Kila sadaka ya nafaka unayoleta
kwa BWANA ni lazima ifanywe bila
kutiwa chachu, kwa kuwa huna ruhusa
kuchoma chachu yoyote au asali katika
sadaka itolewayo kwa BWANA kwa moto.
12 [j]Unaweza kuzileta kwa BWANA kama
sadaka ya malimbuko, lakini haziwezi
kutolewa juu ya madhabahu kama harufu
nzuri ya kupendeza. 13 [k]Koleza sadaka
zako zote za nafaka kwa chumvi. Usiache
kuweka chumvi ya Agano la Mungu wako
katika sadaka zako za nafaka; weka chumvi
kwenye sadaka zako zote.
14 [l]“ ‘Kama ukileta malimbuko ya sadaka
ya nafaka kwa BWANA, utatoa masuke
yaliyopondwa ya nafaka mpya iliyookwa
kwa moto. 15 Weka mafuta na uvumba
juu yake; ni sadaka ya nafaka. 16 [m]Kuhani
atateketeza ile sehemu ya kumbukumbu
kutoka kwenye hiyo sadaka ya nafaka
iliyopondwa kwa mafuta, pamoja na
uvumba wote, kama sadaka iliyotolewa
kwa BWANA kwa moto.

*Sadaka Ya Amani*

3 [n]“ ‘Kama sadaka ya mtu ni sadaka ya
amani, naye akatoa ng’ombe kutoka
kundi, akiwa dume au jike, atamleta
mnyama asiye na dosari mbele za BWANA.
2 [o]Ataweka mkono wake juu ya kichwa cha
sadaka yake na kumchinja penye ingilio la
Hema la Kukutania. Ndipo makuhani wana
wa Aroni watanyunyiza damu yake pande
zote za madhabahu. 3 [p]Kutoka kwenye hiyo

[a]**2:1** Kut 29:2, 41; Law 6:14-18; 5:11; 7:12; 24:7; Hes 15:4; 28:5; Neh 13:9; Isa 43:23
[b]**2:2** Law 1:9; 5:11, 12; 6:15; 24:7; Isa 1:13; 53:12; 65:3; 66:3; Hes 5:26; 18:8; Za 16:5; 73:26; Mdo 10:4
[c]**2:3** Law 6:16; 10:12-13; Kut 30:36; Hes 18:9
[d]**2:4** Law 7:9, 12; 8:26; 26:26; Kut 29:2
[e]**2:5** Law 6:21; 7:9; Eze 4:3
[f]**2:7** Law 7:9
[g]**2:9** Mwa 8:21; Kut 29:18; Rum 12:1
[h]**2:10** Ezr 2:63; Kut 29:18, 37
[i]**2:11** Kut 34:25; 23:18; Law 6:16; Mt 16:12; Mk 8:15; 1Kor 5:8; Gal 5:8-9
[j]**2:12** Kut 34:22; 22:29; Law 23:10-11; Kum 26:10
[k]**2:13** Mk 9:49; Hes 18:19; 2Nya 13:5; Eze 43:24; Kol 4:6
[l]**2:14** Kut 34:22; Hes 15:20; Kum 16:13; 26:2; Rut 3:2; Kut 23:19; Mit 3:9; 2Fal 4:42
[m]**2:16** Hes 4:16; Yer 14:12
[n]**3:1** Kut 32:6; 12:5; Law 7:11-34; 17:5
[o]**3:2** Kut 29:15, 20; 40:2; 24:6; Hes 8:10; 18:17; Law 1:5; 17:6; Isa 53:4; Ebr 9:28; 1Pet 2:24; 3:18
[p]**3:3** Kut 29:13; 12:9; 3:4; 29:13; Law 4:9

sadaka ya amani ataleta sadaka iliyotolewa
kwa Bwana kwa moto: mafuta yote ya
mnyama yafunikayo sehemu za ndani,
ama yanayoungana na hizo sehemu za
ndani, 4 figo zote pamoja na mafuta yote
yanayozizunguka karibu na kiuno na yale
yanayofunika ini, ambayo atayaondoa
pamoja na figo. 5 [a]Kisha wana wa Aroni
wataiteketeza juu ya madhabahu, juu ya ile
sadaka ya kuteketezwa iliyoko juu ya kuni
zinazowaka, kama sadaka ya kuteketezwa
kwa moto, harufu nzuri ya kumpendeza
Bwana.

6 [b]" 'Kama akitoa kondoo au mbuzi kutoka
kundi kama sadaka ya amani kwa Bwana,
atamtoa dume au jike asiye na dosari.
7 [c]Kama akimtoa mwana-kondoo, atamleta
mbele za Bwana. 8 [d]Ataweka mkono wake
juu ya kichwa cha sadaka yake, naye
atamchinja mbele ya Hema la Kukutania.
Kisha wana wa Aroni watanyunyiza damu
yake kwenye madhabahu pande zote.
9 [e]Kutoka kwenye hiyo sadaka ya amani
ataleta dhabihu iliyotolewa kwa Bwana
kwa moto: mafuta yake, mafuta yote ya
mkia uliokatwa karibu na uti wa mgongo,
mafuta yote yanayofunika sehemu za ndani
au yale yanayounganika nazo, 10 figo mbili
pamoja na mafuta yanayozizunguka yaliyo
karibu na kiuno na yale yanayofunika ini,
ambayo atayatoa pamoja na figo. 11 [f]Kuhani
ataviteketeza juu ya madhabahu kama
chakula, sadaka iliyotolewa kwa Bwana
kwa moto.

12 [g]" 'Kama sadaka yake ni mbuzi, ataileta
mbele za Bwana. 13 [h]Ataweka mkono wake
juu ya kichwa chake na kumchinja mbele
ya Hema la Kukutania. Kisha wana wa
Aroni watanyunyiza damu yake kwenye
madhabahu pande zote. 14 Kutokana
na ile sadaka anayotoa, atatoa sadaka
hii kwa Bwana kwa moto: mafuta yote
yanayofunika sehemu za ndani na yale
yanayoungana nazo, 15 [i]figo zote mbili
pamoja na mafuta yaliyo juu yake karibu
na kiuno na yanayofunika ini, ambayo
atayaondoa pamoja na figo. 16 Kuhani
ataviteketeza juu ya madhabahu kama
chakula, sadaka iliyotolewa kwa moto,
harufu nzuri. Mafuta yote ya mnyama ni
ya Bwana.

17 [j]" 'Hii ni kanuni ya kudumu kwa vizazi
vijavyo, popote muishipo: Msile mafuta
yoyote ya mnyama wala damu.' "

*Sadaka Ya Dhambi*

4 Bwana akamwambia Mose, 2 [k]"Waambie
Waisraeli: 'Mtu yeyote afanyapo dhambi
bila kukusudia na akatenda lile lililokatazwa
katika amri yoyote ya Bwana:

3 [l]" 'Ikiwa kuhani aliyetiwa mafuta
amefanya dhambi na kuwaletea watu
hatia, lazima alete kwa Bwana fahali
mchanga asiye na dosari, kuwa sadaka ya
dhambi kwa ajili ya dhambi aliyotenda.
4 [m]Atamkabidhi huyo fahali kwenye ingilio
la Hema la Kukutania mbele za Bwana.
Ataweka mkono wake juu ya kichwa
cha huyo fahali na kumchinja mbele za
Bwana. 5 [n]Kisha kuhani huyo aliyetiwa
mafuta atachukua sehemu ya damu ya huyo
fahali na kuileta katika Hema la Kukutania.
6 [o]Atachovya kidole chake katika hiyo damu
na kuinyunyiza sehemu yake mara saba
mbele za Bwana mbele ya pazia la mahali

[a]**3:5** Law 1:7-9; 7:29-34; Kut 29:13, 38-42; Hes 28:3-10; 1Sam 2:15-16
[b]**3:6** Law 22:21; Hes 15:3, 8; 2Kor 5:21; Tit 2:11-12; Ebr 7:26-27
[c]**3:7** Law 17:3, 8-9; Hes 15:5; 28:5-8; 1Fal 8:62
[d]**3:8** Law 1:5
[e]**3:9** Isa 34:6; Yer 46:10; Eze 39:19; Sef 1:7
[f]**3:11** Law 21:6, 17; 9:18; Hes 28:2; Eze 44:7
[g]**3:12** Law 1:10; 4:3
[h]**3:13** Kut 24:6; Law 1:5
[i]**3:15** Law 7:4; 3:16; 7:31; 1:9; Mwa 4:4; 1Sam 2:16; Law 7:23; 2Nya 7:7
[j]**3:17** Kut 12:14, 20; 27:21; Mwa 9:12; Law 7:25-26; 17:10-16; Kum 12:16; Mdo 15:20
[k]**4:2** Law 5:15-18; 22:14; Hes 15:22, 24-29; 35:11-15; Yos 20:3-9; Ebr 9:4; 1Sam 14:27; Za 19:12
[l]**4:3** Kut 12:5; 28:41; 30:10; Mwa 18:23; Law 3:12; 5:6-13; 9:2-22; 8:14; 10:16; 16:3-5; Hes 15:27; Za 66:15; Eze 43:19-23; Ebr 9:13-14
[m]**4:4** Law 1:3; Hes 8:12; 19:4
[n]**4:5** Law 16:14
[o]**4:6** Kut 24:8; 25:8; Law 16:14-19; Isa 42:21; Yn 8:20; Rum 3:24; 2Kor 5:19; Efe 2:13; Ufu 5:9

patakatifu. 7 [a]Kisha kuhani atatia sehemu
ya hiyo damu juu ya pembe za madhabahu
ya kufukizia uvumba wenye harufu nzuri
iliyoko mbele za Bwana katika Hema la
Kukutania. Damu iliyobaki ya huyo fahali
ataimwaga chini ya hayo madhabahu ya
kuteketezea sadaka kwenye ingilio la Hema
la Kukutania. 8 Atayaondoa mafuta yote ya
fahali huyo wa sadaka ya dhambi, mafuta
yale yanayofunika sehemu za ndani au zile
zinazounganika nazo, 9 [b]figo zote mbili na
mafuta yaliyo juu yake karibu na kiuno na
yale yanayofunika ini ambayo atayaondoa
pamoja na figo zote, 10 [c]kama vile mafuta
yanayoondolewa kutoka kwenye maksai
aliyetolewa sadaka ya amani. Kisha kuhani
ataviteketeza juu ya madhabahu ya sadaka
ya kuteketezwa. 11 [d]Lakini ngozi ya huyo
fahali na nyama zake zote, pamoja na
kichwa na miguu yake, sehemu za ndani
na matumbo, 12 yaani sehemu nyingine zote
zilizobaki za huyo fahali, lazima azitoe nje
ya kambi mpaka mahali palipo safi kiibada,
ambapo majivu hutupwa, naye atamchoma
kwa moto juu ya kuni zilizoko juu ya lundo
la majivu.

13 [e]“ ‘Ikiwa jumuiya yote ya Israeli
watatenda dhambi pasipo kukusudia na
kufanya lile lililokatazwa katika amri
yoyote ya Bwana, hata kama jumuiya
haifahamu juu ya jambo hilo, wana
hatia. 14 [f]Wanapotambua kuhusu dhambi
waliyoitenda, lazima kusanyiko lilete
fahali mchanga kuwa sadaka ya dhambi
na kuikabidhi mbele ya Hema la Kukutania.
15 Wazee wa jumuiya wataweka mikono yao
juu ya kichwa cha huyo fahali aliye mbele
za Bwana, naye fahali atachinjwa mbele za
Bwana. 16 Kisha kuhani aliyetiwa mafuta
ataiingiza sehemu ya damu ya huyo fahali
ndani ya Hema la Kukutania. 17 [g]Atachovya
kidole chake kwenye damu na kuinyunyiza
mara saba mbele za Bwana mbele ya hilo
pazia. 18 [h]Atatia sehemu ya hiyo damu juu
ya pembe za madhabahu yaliyo mbele za
Bwana katika Hema la Kukutania. Damu
iliyobaki ataimwaga chini ya madhabahu
ya kuteketezea sadaka, penye ingilio la
Hema la Kukutania. 19 Atayaondoa mafuta
yote ya yule fahali na kuyateketeza juu
ya madhabahu, 20 [i]naye atamfanyia fahali
huyu kama alivyomfanyia yule fahali
mwingine wa sadaka ya dhambi. Kwa njia
hii kuhani atawafanyia watu upatanisho,
nao watasamehewa. 21 [j]Kisha atamchukua
yule fahali nje ya kambi na kumteketeza
kama alivyomteketeza yule wa kwanza. Hii
ni sadaka ya dhambi kwa ajili ya jumuiya.

22 [k]“ ‘Wakati kiongozi ametenda dhambi
bila kukusudia na kufanya yaliyokatazwa
katika amri yoyote ya Bwana Mungu
wake, ana hatia. 23 [l]Atakapofahamishwa
dhambi aliyotenda, ni lazima alete mbuzi
dume asiye na dosari kama sadaka yake.
24 [m]Ataweka mkono wake juu ya kichwa
cha yule mbuzi na kumchinja mahali pale
ambapo sadaka za kuteketezwa huchinjiwa
mbele za Bwana. Hii ni sadaka ya dhambi.
25 [n]Kisha kuhani atachukua sehemu ya damu
ya sadaka ya dhambi kwa kidole chake
na kuitia kwenye pembe za madhabahu
ya sadaka ya kuteketeza, na kuimwaga
damu iliyobaki chini ya madhabahu.
26 [o]Atayateketeza mafuta yote juu ya
madhabahu, kama alivyoteketeza mafuta
ya sadaka ya amani. Kwa njia hii kuhani
atafanya upatanisho wa dhambi kwa ajili
ya yule mtu, naye atasamehewa.

---

[a]**4:7** Kut 27:2; 29:12; Law 8:15; 5:9; 9:9; 16:18; Ebr 9:21-25; Yos 7:11
[b]**4:9** Law 3:4
[c]**4:10** Kut 32:2; 29:13
[d]**4:11** Kut 29:14; Law 8:17; 9:11; Hes 19:5; 4:12; Kut 29:14; Law 1:16; 6:11, 30; 8:17; 9:11; 10:14; Ebr 13:11; Hes 19:9
[e]**4:13** Hes 15:24-26
[f]**4:14** Hes 15:24; 4:15; Kut 3:16; 19:7; 29:10; 2Nya 29:23; Hes 8:10; Isa 53:6; Mt 8:17; Ebr 9:2; 9:12-14
[g]**4:17** Hes 19:4, 18
[h]**4:18** Law 5:9; 6:30; 8:15; 10:18; 17:6; 2Nya 29:22
[i]**4:20** Kut 29:36; 32:30; Rum 3:25; Ebr 10:10-15; Hes 15:25; Dan 9:24
[j]**4:21** Law 16:5, 15; 2Nya 29:21
[k]**4:22** Hes 31:13
[l]**4:23** Law 1:10; Kut 18:21; Hes 16:2; Ezr 9:2; Mdo 3:17; 2Sam 21:1-3
[m]**4:24** Law 6:25
[n]**4:25** Law 9:9; 16:18; Eze 43:20-22
[o]**4:26** Kut 32:30; Law 5:10; 12:8; Hes 15:28

27 [a]“ ‘Kama mtu katika jumuiya ametenda dhambi pasipo kukusudia na kufanya lile lililokatazwa katika amri yoyote ya BWANA, yeye ana hatia.
28 [b]Atakapofahamishwa dhambi yake aliyoitenda, ni lazima alete mbuzi jike asiye na dosari kama sadaka yake kwa ajili ya dhambi aliyotenda.
29 [c]Ataweka mkono wake juu ya kichwa cha sadaka ya dhambi na kumchinjia mahali pa kuteketezea sadaka.
30 Kisha kuhani atachukua sehemu ya ile damu kwa kidole chake na kuitia kwenye pembe za madhabahu ya sadaka ya kuteketezwa na kuimwaga damu iliyobaki chini ya madhabahu.
31 [d]Atayaondoa mafuta yote, kama vile mafuta yaondolewavyo kwenye sadaka ya amani, naye kuhani atayateketeza juu ya madhabahu kama harufu nzuri ya kumpendeza BWANA. Kwa njia hii kuhani atafanya upatanisho kwa ajili yake, naye atasamehewa.

32 [e]“ ‘Ikiwa ataleta mwana-kondoo kama sadaka yake ya dhambi, atamleta jike asiye na dosari.
33 Ataweka mkono wake juu ya kichwa cha huyo mwana-kondoo na kumchinja kwa ajili ya sadaka ya dhambi mahali sadaka ya kuteketezwa huchinjiwa.
34 Kisha kuhani atachukua sehemu ya damu ya sadaka ya dhambi kwa kidole chake na kuitia juu ya pembe za madhabahu ya sadaka ya kuteketezwa, na ile damu iliyobaki ataimwaga chini ya madhabahu.
35 Ataondoa mafuta yote, kama vile mafuta yaondolewavyo kutoka kwenye mwana-kondoo wa sadaka ya amani, naye kuhani atayateketeza juu ya madhabahu juu ya zile sadaka zilizotolewa kwa BWANA kwa moto. Kwa njia hii kuhani atafanya upatanisho kwa ajili yake kwa dhambi aliyoitenda, naye atasamehewa.

[a]**4:27** Hes 15:27
[b]**4:28** Eze 40:39; 44:27; Law 1:10
[c]**4:29** Law 1:4; Mwa 8:21
[d]**4:31** Mwa 8:21; Law 1:4; 3:14; Kut 29:18; Ezr 6:10
[e]**4:32** Kut 29:38; Law 9:3; 14:10; 1:3-4; Isa 53:7; Yn 1:29; Mdo 8:32; Ufu 5:6-14

*Sadaka Zingine Za Kuondoa Dhambi*

5 [f]“ ‘Ikiwa mtu atakuwa ametenda dhambi kwa sababu hakusema alipotakiwa kutoa ushahidi hadharani kuhusu jambo aliloona au kujua habari zake, yeye anastahili adhabu.

2 [g]“ ‘Au kama mtu akigusa kitu chochote ambacho ni najisi, iwe ni mizoga ya wanyama pori walio najisi, au ya wanyama wafugwao walio najisi, au ya viumbe vitambaavyo ardhini, hata akiwa hana habari, amekuwa najisi na mwenye hatia.

3 [h]“ ‘Au kama akigusa kitu kilicho kichafu kinachotokana na binadamu, kitu chochote kile kinachoweza kumfanya awe najisi, hata akiwa hana habari, atakapofahamu atakuwa na hatia.

4 [i]“ ‘Au kama mtu ameapa kufanya kitu chochote bila kufikiri, kiwe chema au kibaya, kwa vyovyote mtu aweza kuapa bila kujali, hata akiwa hana habari, atakapofahamu atakuwa na hatia.

5 [j]“ ‘Wakati mtu yeyote atakapokuwa na hatia katika mojawapo ya haya, lazima akiri ni kwa njia gani ametenda dhambi,
6 [k]na kama adhabu ya dhambi aliyoitenda, lazima alete kwa BWANA kondoo jike au mbuzi jike kutoka kwenye kundi lake kama sadaka ya dhambi; naye kuhani atafanya upatanisho kwa ajili yake kwa dhambi yake.

7 [l]“ ‘Lakini huyo mtu kama hataweza kumtoa mwana-kondoo, ataleta hua wawili au makinda mawili ya njiwa kwa BWANA kuwa adhabu kwa ajili ya dhambi yake, mmoja wa hao ndege kwa ajili ya

[f]**5:1** Mit 29:24; Mt 26:63; Kut 28:38; Law 7:18; 17:16; 19:8; 20:17; 24:15; Hes 5:31; 9:15; 15:31; 19:20; 30:15
[g]**5:2** Law 7:21; 11:8, 11, 24-40; 13:45; Kum 14:8; Isa 6:5; 52:11; 64:5; Hes 19:22; Ay 15:16; Za 51:5; Eze 36:17; Hag 2:13
[h]**5:3** Hes 5:2; 9:6; 19:7, 11-16; Law 7:20; 11:25; 14:19; 21:1; Eze 44:25
[i]**5:4** Isa 41:23; 1Sam 14:24; 25:22; Mdo 23:12; Mk 6:23
[j]**5:5** Law 16:21; 26:40; Hes 5:7; Yos 7:19; 1Fal 8:47; Mit 28:13
[k]**5:6** Law 1:10; 4:3, 28; Kum 32:30
[l]**5:7** Law 12:8; 14:21-40; 27:8; Mwa 15:9; Hes 6:10

sadaka ya dhambi, na wa pili kwa ajili ya sadaka ya kuteketezwa. 8 [a]Atawaleta kwa kuhani, ambaye atamtoa kwanza ndege mmoja kwa ajili ya sadaka ya dhambi. Atamvunja shingo na kuacha kichwa chake kikining'inia, 9 [b]naye atanyunyiza sehemu ya hiyo damu ya sadaka ya dhambi kwenye pembe za madhabahu. Damu iliyobaki lazima ichuruzwe chini ya madhabahu. Hii ni sadaka ya dhambi. 10 [c]Kisha kuhani atamtoa yule ndege wa pili kama sadaka ya kuteketezwa kwa kufuata utaratibu uliowekwa, na hivyo kufanya upatanisho kwa ajili yake kwa dhambi aliyoitenda, naye atasamehewa.

11 [d]" 'Ikiwa basi, hawezi kupata hua wawili au makinda mawili ya njiwa, ataleta sehemu ya kumi ya efa[e] ya unga laini kwa ajili ya sadaka ya dhambi. Kamwe asiweke mafuta wala uvumba juu yake, kwa sababu ni sadaka ya dhambi. 12 [f]Atauleta unga kwa kuhani, ambaye atachukua konzi moja kama sehemu ya kumbukumbu na atauteketeza kwenye madhabahu juu ya sadaka zilizotolewa kwa BWANA kwa moto. Hii ni sadaka ya dhambi. 13 [g]Kwa njia hii kuhani atafanya upatanisho kwa ajili yake kwa dhambi yoyote ya hizo alizotenda, naye atasamehewa. Sadaka iliyobaki itakuwa ya kuhani, kama ilivyokuwa ile sadaka ya nafaka.' "

*Sadaka Ya Hatia*

14 BWANA akamwambia Mose: 15 [h]"Mtu anapokiuka na kutenda dhambi pasipo kukusudia kuhusu mojawapo ya mambo matakatifu ya BWANA, huyo mtu ataleta kwa BWANA kama adhabu kondoo dume mmoja kutoka kundi lake, asiye na dosari na mwenye thamani halisi kifedha, kulingana na shekeli ya mahali patakatifu. Hii ni sadaka ya hatia. 16 [i]Ni lazima alipe kwa yale aliyoshindwa kufanya kuhusu vitu vitakatifu, kwa kuongeza sehemu ya tano ya thamani ile na kuitoa yote kwa kuhani, ambaye atamfanyia upatanisho kwa huyo kondoo dume kama sadaka ya dhambi, naye atasamehewa.

17 [j]"Kama mtu akifanya dhambi na kufanya yale yaliyokatazwa katika mojawapo ya amri za BWANA, hata ikiwa hajui, yeye ana hatia na anastahili adhabu. 18 [k]Atamletea kuhani kama sadaka ya hatia kondoo dume kutoka kundi lake, kondoo asiye na dosari na mwenye thamani halisi kifedha. Kwa njia hii kuhani atafanya upatanisho kwa ajili yake kwa kosa alilotenda bila kukusudia, naye atasamehewa. 19 [l]Hii ni sadaka ya hatia; amekuwa na hatia kwa kufanya kosa dhidi ya BWANA."

*Kurudisha Kilichochukuliwa*

6 BWANA akamwambia Mose: 2 [m]"Kama mtu yeyote akitenda dhambi, naye si mwaminifu kwa BWANA kwa kumdanganya jirani yake kuhusu kitu fulani alichokabidhiwa, au kimeachwa chini ya utunzaji wake, au kimeibwa, au kama akimdanganya, 3 [n]au akiokota mali iliyopotea na akadanganya, au kuapa kwa uongo, au kama akitenda dhambi yoyote ambayo watu waweza kuitenda; 4 [o]wakati akitenda dhambi hizo na kuwa mwenye hatia, ni lazima arudishe kile alichokuwa amekiiba au amekichukua kwa dhuluma, au alichokuwa amekabidhiwa, au mali

[a]**5:8** Law 1:15-17
[b]**5:9** Kut 24:6; Law 1:15; 4:17
[c]**5:10** Law 1:14-17; 4:26; 1Nya 15:13; Kut 32:30
[d]**5:11** Mwa 15:9; Law 2:1; Kut 16:36; Hes 5:15
[e]11 Sehemu ya kumi ya efa ni sawa na kilo moja.
[f]**5:12** Law 2:2, 9; 4:35
[g]**5:13** Kut 32:30; 29:41; Law 2:3
[h]**5:15** Law 4:2; 6:6; 14:12-17; 19:21-22; 22:14; Kut 29:3; 30:13; Hes 5:8; 6:12, 18; 15:6; 18:9; 28:11; 1Sam 9:3; Eze 10:19; Isa 53:10
[i]**5:16** Law 6:4; 27:13; Hes 5:7; Law 22:14; Ebr 9:13-14
[j]**5:17** Law 4:2; Za 19:12; Lk 12:48
[k]**5:18** Law 6:6; 14:12
[l]**5:19** 2Fal 12:16; Isa 53:10; Ezr 10:2
[m]**6:2** Hes 5:6; Za 73:27; Mdo 5:4; Kol 3:9; Law 19:11; Yer 9:4-5; Kut 22:7; Mwa 31:7; Mit 24:28
[n]**6:3** Kut 23:4; 22:11; Kum 22:1-3; Law 19:12; Yer 7:9; Zek 5:4
[o]**6:4** Law 5:16; Eze 33:15; Lk 19:8

iliyokuwa imepotea akaipata, 5 [a]au chochote
alichokuwa amekiapia kwa uongo. Lazima
akirudishe kikamilifu, na aongeze sehemu
ya tano ya thamani yake, vyote ampe
mwenye mali siku ile anapeleka sadaka
yake ya hatia. 6 [b]Kisha kama adhabu lazima
amletee kuhani, yaani kwa Bwana, kama
sadaka yake ya hatia, kondoo dume asiye na
dosari na mwenye thamani kamili kutoka
kundi lake. 7 [c]Kwa njia hii kuhani atafanya
upatanisho kwa ajili yake mbele za Bwana,
naye atasamehewa kwa kosa lolote katika
mambo hayo aliyoyatenda yaliyomfanya
kuwa na hatia."

*Sadaka Ya Kuteketezwa*

8 Bwana akamwambia Mose: 9 [d]"Mpe
Aroni na wanawe agizo hili: 'Haya ndiyo
masharti kwa ajili ya sadaka ya kuteketezwa:
Sadaka ya kuteketezwa itabaki kwenye
moto juu ya madhabahu usiku kucha,
mpaka asubuhi, nao moto lazima uwe
unaendelea kuwaka juu ya madhabahu.
10 [e]Kisha kuhani atavaa mavazi yake ya
kitani, pamoja na nguo za ndani za kitani
mwilini wake, na aondoe majivu ya sadaka
ya kuteketezwa ambayo moto umeteketeza
juu ya madhabahu, na kuyaweka kando
ya madhabahu. 11 [f]Kisha atayavua mavazi
haya na kuvaa mengine, naye achukue
yale majivu nje ya kambi na kuyapeleka
mahali palipo safi kwa kawaida ya ibada.
12 [g]Moto ulio juu ya madhabahu lazima uwe
unaendelea kuwaka, kamwe usizimike. Kila
asubuhi kuhani ataongeza kuni na kupanga
sadaka ya kuteketezwa juu ya moto, na
kuteketeza mafuta ya sadaka za amani juu
yake. 13 [h]Moto lazima uendelee kuwaka juu
ya madhabahu mfululizo, kamwe usizimike.

*Sadaka Ya Nafaka*

14 [i]" 'Haya ndiyo masharti ya sadaka ya
nafaka: Wana wa Aroni wataileta mbele za
Bwana, mbele za madhabahu. 15 [j]Kuhani
atachukua konzi ya unga laini na mafuta,
pamoja na uvumba wote ulioko juu ya
sadaka ya nafaka, ateketeze sehemu ya
kumbukumbu juu ya madhabahu kama
harufu nzuri ya kumpendeza Bwana.
16 [k]Aroni na wanawe watakula sehemu
iliyobaki, lakini italiwa bila kutiwa chachu
mahali patakatifu, nao wataila kwenye
ua wa Hema la Kukutania. 17 [l]Kamwe
haitaokwa na chachu; nimewapa kama
fungu lao la sadaka iliyotolewa kwangu
kwa moto. Ni takatifu sana, kama vile
ilivyo sadaka ya dhambi na ya hatia.
18 [m]Kila mwanaume mzao wa Aroni aweza
kuila. Ni fungu lake la kawaida la sadaka
zilizotolewa kwa Bwana kwa moto kwa
vizazi vijavyo. Chochote kinachozigusa
kitakuwa kitakatifu.' "

19 Tena Bwana akamwambia Mose,
20 [n]"Hii ni sadaka ambayo Aroni na
wanawe wanapaswa kuleta kwa Bwana
siku atakapotiwa mafuta: sehemu ya
kumi ya efa[o] ya unga laini kama sadaka
ya kawaida ya nafaka. Nusu yake ataitoa
asubuhi na nusu nyingine jioni. 21 [p]Iandae
kwa mafuta kwenye kikaango; ilete ikiwa
imechanganywa vizuri, na utoe hiyo
sadaka ya nafaka ikiwa imevunjwa vipande
vipande kuwa harufu nzuri ya kumpendeza
Bwana. 22 Mwanawe atakayeingia mahali
pake kama kuhani aliyetiwa mafuta ndiye
atakayeiandaa. Ni fungu la kawaida la
Bwana, nalo litateketezwa kabisa. 23 Kila

---

[a]**6:5** Hes 5:7; Law 5:15; 2Sam 12:6; Lk 19:8
[b]**6:6** Law 5:15; Hes 5:8; Kut 12:5; Kum 15:21; Efe 5:27; Ebr 9:14; 10:1-17
[c]**6:7** Kut 32:30; Law 4:26
[d]**6:9** Law 7:37
[e]**6:10** Kut 39:27, 28; 28:39-43; Law 1:16; Eze 44:17
[f]**6:11** Law 4:12
[g]**6:12** Law 1:7; Kut 29:13; 32:6
[h]**6:13** Isa 33:14; Dan 7:10; Mt 25:41
[i]**6:14** Law 2:1; Hes 6:15; 15:4; 28:13
[j]**6:15** Law 2:1, 9
[k]**6:16** Law 2:2-3, 11; 8:31; 10:13; 16:24; 24:9; Eze 44:29; Kut 27:9; 29:11, 31; Hes 18:10
[l]**6:17** Hes 5:9; 18:9-10; Kut 29:28; 40:10; Law 7:7; 10:12; 21:22
[m]**6:18** Law 2:3; 7:6; Hes 18:9-10; 5:9; Mwa 9:12; Kut 30:29
[n]**6:20** Kut 28:41; 16:36; 29:2; Hes 4:16; 5:15; 28:5; Law 23:13
[o]20 Sehemu ya kumi ya efa ni sawa na kilo moja.
[p]**6:21** Law 2:5; 6:22; Kut 28:41; 29:30; Law 1:9; Isa 53:10; Mt 20:28; Dan 9:26

sadaka ya nafaka ya kuhani itateketezwa
kabisa; kamwe haitaliwa.”

*Sadaka Ya Dhambi*

24 BWANA akamwambia Mose,
25 [a]“Mwambie Aroni na wanawe: ‘Haya
ndiyo masharti kwa ajili ya sadaka ya
dhambi: Sadaka ya dhambi itachinjiwa
mbele za BWANA mahali sadaka ya
kuteketezwa huchinjiwa, ni takatifu sana.
26 [b]Kuhani anayeitoa ndiye atakayeikula;
itakuliwa katika mahali patakatifu, katika
ua wa Hema la Kukutania. 27 [c]Chochote
kitakachogusa nyama yoyote ya hiyo sadaka
kitakuwa kitakatifu, na kama hiyo damu
itadondokea juu ya vazi, lazima uifulie
mahali patakatifu. 28 [d]Chungu cha udongo
kitakachopikiwa nyama lazima kivunjwe,
lakini kama imepikiwa kwenye chombo
cha shaba, chombo hicho kitasuguliwa na
kusuuzwa kwa maji. 29 [e]Kila mwanaume
katika familia ya kuhani aweza kula nyama
hiyo; ni takatifu sana. 30 [f]Lakini kila sadaka
ya dhambi ambayo damu yake imeletwa
ndani ya Hema la Kukutania kufanya
upatanisho katika Mahali Patakatifu kamwe
haitaliwa; lazima iteketezwe.

*Sadaka Ya Hatia*

7 [g]“ ‘Haya ndiyo masharti kwa ajili ya
sadaka ya hatia, ambayo ni takatifu
sana: 2 Sadaka ya hatia itachinjiwa mahali
pale ambapo sadaka ya kuteketezwa
huchinjiwa, nayo damu yake itanyunyizwa
pande zote za madhabahu. 3 [h]Mafuta yake
yote yatatolewa sadaka: mafuta ya mkia
na mafuta yale yanayofunika sehemu
za ndani, 4 [i]figo zote mbili pamoja na
mafuta yanayozizunguka yaliyo karibu na
kiuno na yale yanayofunika ini, ambayo
yataondolewa pamoja na hizo figo.
5 [j]Kuhani atayateketeza juu ya madhabahu
kuwa sadaka iliyotolewa kwa BWANA kwa
moto. Hii ni sadaka ya hatia. 6 [k]Mwanaume
yeyote katika jamaa ya kuhani aweza kuila,
lakini lazima iliwe mahali patakatifu; ni
takatifu sana.
7 [l]“ ‘Sheria hii ya sadaka ya hatia ni
sawasawa na ile ya sadaka ya dhambi:
Nyama ya yule mnyama aliyetolewa sadaka
ni ya yule kuhani anayesimamia ibada ya
upatanisho. 8 Kuhani anayetoa sadaka
ya kuteketezwa kwa ajili ya mtu yeyote
anaweza kuichukua ngozi ya mnyama
yule aliyetolewa iwe yake. 9 [m]Kila sadaka
ya nafaka iliyookwa jikoni au kupikwa
katika sufuria au katika kikaangio itakuwa
ya kuhani anayeitoa. 10 Nayo kila sadaka ya
nafaka, iwe imechanganywa na mafuta au
iko kavu, itakuwa ya wana wa Aroni, nayo
itagawanywa sawa kati yao.

*Sadaka Ya Amani*

11 “ ‘Haya ndiyo masharti kwa ajili ya
sadaka ya amani ambayo mtu aweza kuileta
kwa BWANA:
12 [n]“ ‘Ikiwa mtu atatoa sadaka ya amani
kwa ajili ya kuonyesha shukrani, pamoja
na sadaka hii ya shukrani, atatoa maandazi
yasiyotiwa chachu yaliyochanganywa na
mafuta, mikate myembamba isiyotiwa
chachu iliyopakwa mafuta, maandazi
ya unga laini uliokandwa vizuri na
kuchanganywa na mafuta. 13 [o]Pamoja na
sadaka hii ya amani ya shukrani ataleta
sadaka ya maandazi yaliyotengenezwa kwa

---

[a]**6:25** Kut 29:11; 30:10; Law 4:24; 1:3; Za 93:5
[b]**6:26** Kut 27:9, 21; 40:2; Hes 18:9; Eze 44:27-28
[c]**6:27** Kut 29:37; Law 10:10; Eze 44:19; 46:20; Hag 2:12
[d]**6:28** Law 11:33; 15:12; Hes 19:15
[e]**6:29** Eze 42:13
[f]**6:30** Eze 45:15; Law 4:12, 18; 16:27; Ebr 13:11
[g]**7:1** Law 5:15; Eze 40:39; Kut 29:27; Law 6:17; 21:22
[h]**7:3** Kut 29:13; Law 3:4-9
[i]**7:4** Law 3:15
[j]**7:5** Kut 29:13; Tit 2:14; Ebr 9:28
[k]**7:6** Law 6:18; Eze 42:13; Law 3:3; Za 93:5; Law 14:13
[l]**7:7** Kut 30:10; Law 5:15; 2:3; 6:17; 14:13; 2Fal 12:16; 1Kor 9:13; 10:18; Hes 5:8
[m]**7:9** Law 2:4-7; Hes 18:9; Eze 44:29
[n]**7:12** Law 2:1-4; 22:29; Za 50:14; 54:6; 107:22; 116:17; Yer 33:11; 44:19; Hes 6:19
[o]**7:13** Kut 34:22; Law 23:17; Amo 4:5

chachu. 14 [a]Ataleta moja ya kila aina ya
andazi kama sadaka, matoleo kwa BWANA;
hii ni ya kuhani anayenyunyiza damu ya
sadaka ya amani. 15 [b]Nyama ya sadaka ya
amani kwa ajili ya shukrani lazima iliwe
siku iyo hiyo inapotolewa; hutabakiza kitu
chochote mpaka asubuhi.

16 [c]“ ‘Lakini kama sadaka yake ni kwa ajili
ya nadhiri au ni sadaka ya hiari, sadaka
hiyo italiwa siku hiyo inapotolewa, lakini
chochote kinachobakia kinaweza kuliwa
kesho yake. 17 [d]Nyama yoyote ya sadaka
inayobaki mpaka siku ya tatu lazima
iteketezwe kwa moto. 18 [e]Kama nyama
yoyote ya sadaka ya amani italiwa siku ya
tatu, BWANA hataikubali. Haitahesabiwa
kwake huyo aliyeitoa, kwa kuwa ni najisi.
Mtu atakayekula sehemu yake yoyote
atahesabiwa hatia.

19 “ ‘Nyama ile inayogusa chochote
ambacho ni najisi kwa kawaida ya ibada
kamwe haitaliwa, ni lazima iteketezwe kwa
moto. Kuhusu nyama nyingine, mtu yeyote
aliye safi kwa kawaida ya ibada anaweza
kuila. 20 [f]Lakini kama mtu yeyote najisi
akila nyama yoyote ya sadaka ya amani
iliyotolewa kwa BWANA, huyo mtu lazima
akatiliwe mbali na watu wake. 21 [g]Kama mtu
yeyote akigusa kitu kilicho najisi, iwe ni
uchafu wa mwanadamu, au mnyama najisi,
au kitu chochote kilicho najisi, kitu cha
kuchukiza, kisha akala nyama yoyote ya
sadaka ya amani iliyotolewa kwa BWANA,
mtu huyo ni lazima akatiliwe mbali na watu
wake.’ ”

*Kula Mafuta Na Kunywa Damu Kwakatazwa*

22 BWANA akamwambia Mose,
23 [h]“Waambie Waisraeli: ‘Msile mafuta
yoyote ya ng’ombe, kondoo wala mbuzi.
24 [i]Mafuta ya mnyama aliyekutwa amekufa
au ameraruliwa na mnyama pori yanaweza
kutumika kwa kazi nyingine yoyote,
lakini kamwe msiyale. 25 Mtu yeyote alaye
mafuta ya mnyama ambaye ametolewa
sadaka kwa BWANA kwa moto ni lazima
akatiliwe mbali na watu wake. 26 [j]Popote
mtakapoishi, kamwe msinywe damu ya
ndege yeyote wala ya mnyama. 27 [k]Ikiwa
mtu yeyote atakunywa damu, mtu huyo
lazima akatiliwe mbali na watu wake.’ ”

*Fungu La Makuhani*

28 BWANA akamwambia Mose,
29 “Waambie Waisraeli: ‘Mtu yeyote aletaye
sadaka ya amani kwa BWANA ataleta
sehemu ya sadaka hiyo kama dhabihu
yake kwa BWANA. 30 [l]Ataleta sadaka kwa
mikono yake mwenyewe iliyotolewa kwa
BWANA kwa moto; ataleta mafuta ya huyo
mnyama pamoja na kidari, naye atainua
hicho kidari mbele za BWANA kuwa sadaka
ya kuinuliwa. 31 [m]Kuhani atayateketeza hayo
mafuta juu ya madhabahu, lakini kidari
kitakuwa cha Aroni na wanawe. 32 [n]Paja
la kulia la sadaka zako za amani utampa
kuhani kama matoleo. 33 Mwana wa Aroni
atoaye damu na mafuta ya sadaka ya amani
ndiye atakayepewa paja hilo la kulia kuwa
fungu lake. 34 [o]Kutoka kwenye sadaka za
amani za Waisraeli, mimi Mungu nimepokea
kidari kile kilichoinuliwa pamoja na lile
paja lililotolewa, nami nimevitoa kwa
kuhani Aroni na wanawe kuwa fungu lao
la kawaida kutoka kwa Waisraeli.’ ”

35 Hii ndiyo sehemu ya sadaka
zilizotolewa kwa BWANA kwa moto, ambazo

---

[a]**7:14** Hes 18:8
[b]**7:15** Kut 12:10; Law 22:30; Ebr 3:13-15
[c]**7:16** Mwa 28:20; Kum 12:6; 23:21-23; Kut 35:29; Law 19:5-9; 22:18-21; 23:38; Hes 15:3; 29:39; Za 54:6; Eze 46:12
[d]**7:17** Kut 12:10; Law 19:6
[e]**7:18** 2Nya 33:16; Law 5:1; 19:7; Hes 18:27; Mwa 4:4-5; Mit 15:8; 21:27; Yer 6:20; Amo 5:22
[f]**7:20** Law 5:3; 22:3-7; Mwa 17:14; Law 15:3
[g]**7:21** Law 5:2; 11:24-28; 11:10-13; Kum 14:3; Eze 4:14
[h]**7:23** Law 17:13; Kum 14:4; 1Sam 2:29
[i]**7:24** Kut 22:31
[j]**7:26** Mwa 9:4; Law 3:17; 17:10-14; Kum 12:16; 1Sam 14:33; Eze 44:15; Mdo 15:20
[k]**7:27** Mwa 9:4; Mdo 15:20-29
[l]**7:30** Kut 29:24; Hes 6:20; Law 8:27; 9:21
[m]**7:31** Kut 29:27, 31
[n]**7:32** Kut 29:27; Law 10:14-15; Hes 5:9; 6:20; 18:18
[o]**7:34** Kut 29:22, 27; Law 10:15; Hes 6:20; 18:18-19; 1Sam 9:24

zilitengwa kwa ajili ya Aroni na wanawe
siku ile walipowekwa wakfu ili kumtumikia
BWANA katika kazi ya ukuhani. 36 [a]Siku
ile walipotiwa mafuta, BWANA aliagiza
kwamba Waisraeli wawape hili kama fungu
lao la kawaida kwa vizazi vijavyo.

37 [b]Basi haya ndiyo masharti kuhusu
sadaka ya kuteketezwa, sadaka ya nafaka,
sadaka ya dhambi, sadaka ya hatia, sadaka
ya kuwekwa wakfu, na sadaka ya amani,
38 [c]ambayo BWANA alimpa Mose juu ya
Mlima Sinai siku ile alipowaagiza Waisraeli
walete sadaka zao kwa BWANA, katika
Jangwa la Sinai.

*Kuwekwa Wakfu Kwa Aroni Na Wanawe*

**(Kutoka 29:1-37)**

8 BWANA akamwambia Mose, 2 [d]"Waletee
Aroni na wanawe mavazi yao, mafuta
ya upako, fahali kwa ajili ya sadaka ya
dhambi, kondoo dume wawili na kikapu
chenye mikate iliyotengenezwa bila chachu.
3 [e]Kisha kusanya mkutano wote kwenye
ingilio la Hema la Kukutania." 4 Mose
akafanya kama BWANA alivyomwagiza,
na mkutano ukakusanyika kwenye ingilio
la Hema la Kukutania.

5 Mose akaliambia kusanyiko, "Hili
ndilo BWANA ameagiza lifanyike." 6 [f]Kisha
Mose akamleta Aroni na wanawe mbele,
akawaosha kwa maji. 7 [g]Akamvika Aroni
koti, akamfunga mshipi, akamvika joho na
kumvalisha kisibau. Pia akafunga kisibau
juu yake na kukifunga kiunoni mwake
kwa mshipi wake uliosokotwa kwa ustadi.
8 [h]Akaweka kifuko cha kifuani juu yake, na
kuweka Urimu na Thumimu[i] kwenye hicho
kifuko. 9 [j]Kisha akamvika Aroni kilemba
kichwani pake, akaweka lile bamba la
dhahabu, yaani ile taji takatifu, upande
wa mbele wa kilemba, kama BWANA
alivyomwagiza Mose.

10 [k]Ndipo Mose akachukua mafuta
ya upako na kuipaka maskani na kila
kitu kilichokuwamo ndani yake, kisha
akaviweka wakfu. 11 [l]Akanyunyiza baadhi
ya mafuta juu ya madhabahu mara saba,
akaipaka madhabahu mafuta na vyombo
vyake vyote pamoja na sinia na kinara
chake, ili kuviweka wakfu. 12 [m]Akamimina
sehemu ya hayo mafuta ya upako kichwani
mwa Aroni, akamtia mafuta ili kumweka
wakfu. 13 Kisha akawaleta wana wa Aroni
mbele, akawavika makoti, akawafunga
mishipi na kuwavika vilemba, kama BWANA
alivyomwagiza Mose.

14 [n]Kisha akamtoa fahali kwa ajili ya
sadaka ya dhambi, nao Aroni na wanawe
wakaweka mikono yao juu ya kichwa
chake. 15 [o]Mose akamchinja yule fahali
na akachukua sehemu ya hiyo damu,
kisha kwa kidole chake akaitia kwenye
pembe zote za madhabahu ili kutakasa
madhabahu. Akaimwaga damu iliyobaki
chini ya madhabahu. Kwa hiyo akayaweka
wakfu ili kufanya upatanisho kwa ajili ya
madhabahu. 16 [p]Pia Mose akachukua mafuta
yote yanayozunguka sehemu za ndani,
mafuta yanayofunika ini, figo zote mbili
pamoja na mafuta yake, akayateketeza

---

[a]**7:36** Law 8:12, 30; Kut 40:13-15; Ebr 7:18-28; 8:1-13
[b]**7:37** Law 6:9, 14; Kut 29:31; Law 6:20
[c]**7:38** Law 26:46; Hes 36:13; Kum 4:5; 29:1-3; Kut 19:11
[d]**8:2** Kut 28:1-4, 43; 30:10, 23-30; 39:27; 29:2-3; Law 1:5
[e]**8:3** Hes 8:9
[f]**8:6** Kut 29:4; 30:19; Mdo 22:16; Za 26:6; 1Kor 6:11; Isa 52:11; Eze 36:25; Efe 5:26; Ebr 9:9-14
[g]**8:7** Kut 28:4
[h]**8:8** Kut 25:7; 28:30; Hes 27:21; Kum 33:8; 1Sam 28:6; Neh 7:65

[i]8 Urimu na Thumimu maana yake ni Nuru na Kweli; vifaa hivi viliwekwa kwenye kifuko cha juu cha kisibau cha kuhani mkuu ili kujua mapenzi ya Mungu kwenye mambo ya kutatanisha.
[j]**8:9** Kut 39:28; 28:2, 36; Law 21:10; Kut 29:6; Zek 3:5; 6:11
[k]**8:10** Kut 30:26; 26:1
[l]**8:11** Kut 30:29
[m]**8:12** Law 7:36; 21:10-12; Kut 30:30; 29:7; Za 133:2; Isa 61:2; 8:13; Kut 28:4; Law 21:10; Za 132:9; Isa 61:10
[n]**8:14** Law 4:3, 15; Kut 30:10; 29:10; Za 51:19; Eze 43:19; Ebr 9:13-14
[o]**8:15** Law 4:7, 18; Ebr 9:22; Eze 43:20
[p]**8:16** Kut 29:13; Law 4:8; 8:17; 4:11-12; Kut 29:14

juu ya madhabahu. 17 Lakini fahali, ikiwa
pamoja na ngozi yake na nyama yake
na sehemu zake za ndani na matumbo,
akaiteketeza nje ya kambi, kama Bwana
alivyomwagiza Mose.

18 [a]Kisha Mose akamleta kondoo dume
kwa ajili ya sadaka ya kuteketezwa, naye
Aroni na wanawe wakaweka mikono yao juu
ya kichwa chake. 19 Ndipo Mose akamchinja
yule kondoo dume na kunyunyiza damu
yake pande zote za madhabahu. 20 Mose
akamkata yule kondoo dume vipande
vipande na kukiteketeza kichwa,
vile vipande na yale mafuta. 21 Kisha
akamsafisha sehemu za ndani na miguu kwa
maji, na kumteketeza yule kondoo dume
mzima juu ya madhabahu kuwa sadaka ya
kuteketezwa, harufu nzuri ya kupendeza,
sadaka iliyotolewa kwa Bwana kwa moto,
kama Bwana alivyomwagiza Mose.

22 Kisha akaleta kondoo dume mwingine,
ndiye kondoo dume kwa ajili ya kuwaweka
wakfu, naye Aroni na wanawe wakaweka
mikono yao juu ya kichwa chake. 23 [b]Mose
akamchinja yule kondoo dume, akaichukua
sehemu ya damu yake na kuipaka juu ya
ncha ya sikio la kuume la Aroni, na juu ya
kidole gumba cha mkono wake wa kuume
na juu ya kidole kikubwa cha mguu wake
wa kuume. 24 [c]Pia Mose akawaleta hao wana
wa Aroni mbele, akaipaka sehemu ya hiyo
damu kwenye ncha za masikio yao ya kuume,
juu ya vidole gumba vya mikono yao ya
kuume, na juu ya vidole vikubwa vya miguu
yao ya kuume. Kisha akanyunyiza damu
pande zote za madhabahu. 25 [d]Akachukua
mafuta ya mnyama, mafuta ya mkia, mafuta
yote yanayozunguka sehemu za ndani,
mafuta yanayofunika ini, figo zote mbili
pamoja na mafuta yake, na paja la kulia.
26 [e]Kisha kutoka kwenye kikapu cha mikate
iliyotengenezwa bila chachu, kilichokuwa
mbele za Bwana, akachukua andazi moja,
na jingine lililotengenezwa kwa mafuta, na
mkate mwembamba; akaviweka hivi vyote
juu ya mafungu ya mafuta ya mnyama, na
juu ya lile paja la kulia. 27 [f]Akaviweka hivi
vyote mikononi mwa Aroni na wanawe, na
kuviinua mbele za Bwana kuwa sadaka
ya kuinuliwa. 28 [g]Kisha Mose akavichukua
kutoka mikononi mwao na kuviteketeza juu
ya madhabahu ya sadaka ya kuteketezwa
kuwa sadaka ya kuwekwa wakfu, harufu
nzuri ya kupendeza, sadaka iliyotolewa
kwa Bwana kwa moto. 29 [h]Kisha akachukua
kidari, kilicho fungu la Mose la kondoo
dume kwa ajili ya kuwekwa wakfu, na
kukiinua mbele za Bwana kama sadaka
ya kuinuliwa, kama Bwana alivyomwagiza
Mose.

30 [i]Kisha Mose akachukua sehemu ya
mafuta ya upako, na sehemu ya damu kutoka
kwenye madhabahu, na kuvinyunyiza juu
ya Aroni na mavazi yake, na juu ya wanawe
na mavazi yao. Kwa hiyo akamweka Aroni
na mavazi yake wakfu, pamoja na wanawe
na mavazi yao.

31 [j]Kisha Mose akamwambia Aroni
na wanawe, "Pika hiyo nyama kwenye
ingilio la Hema la Kukutania, na uile
hapo pamoja na mkate kutoka kwenye
kikapu cha sadaka ya kuweka wakfu,
kama nilivyoagiza, nikisema, 'Aroni na
wanawe wataila.' 32 Kisha teketeza nyama
na mikate iliyobaki. 33 [k]Msitoke kwenye
ingilio la Hema la Kukutania kwa muda
wa siku saba, mpaka siku zenu za kuwekwa
wakfu ziwe zimetimia, kwa kuwa muda
wenu wa kuwekwa wakfu utakuwa siku
saba. 34 [l]Lile lililofanyika leo liliagizwa
na Bwana ili kufanya upatanisho kwa
ajili yenu. 35 Lazima mkae kwenye ingilio

[a]**8:18** Kut 29:15; 8:22; Law 4:15; Kut 29:19, 31; Law 7:37
[b]**8:23** Law 14:14, 25; 8:23; Rum 12:1; 1Kor 6:20
[c]**8:24** Ebr 9:18-22
[d]**8:25** Law 3:3-5; Kut 29:22
[e]**8:26** Law 2:4
[f]**8:27** Hes 5:25
[g]**8:28** Kut 29:25; Mwa 8:21; Efe 5:2
[h]**8:29** Law 7:31-34
[i]**8:30** Kut 28:1-2; Law 7:36; Kut 30:30; Hes 3:3; 1Pet 1:2
[j]**8:31** Law 6:16; Kut 29:31; Eze 46:20
[k]**8:33** Law 14:8; 15:13, 28; Hes 19:11; Eze 43:25
[l]**8:34** Ebr 7:16; Law 18:30; 22:9; Hes 3:7; 9:19; Kum 11:1; 1Fal 2:3; Eze 48:11; 3:7; 1Tim 5:21

la Hema la Kukutania usiku na mchana
kwa siku saba, na kufanya lile BWANA
analolitaka, ili kwamba msife; kwa kuwa
hilo ndilo nililoamriwa.” 36 Kwa hiyo Aroni
na wanawe wakafanya kila kitu BWANA
alichoamuru kupitia kwa Mose.

*Makuhani Waanza Huduma Yao*

9 [a]Katika siku ya nane, Mose akawaita
Aroni na wanawe, na wazee wa Israeli.
2 [b]Akamwambia Aroni, “Chukua ndama
dume kwa ajili ya sadaka yako ya dhambi,
na kondoo dume kwa sadaka yako ya
kuteketezwa, wote wawili wasiwe na dosari,
nao uwalete mbele za BWANA. 3 [c]Kisha
waambie Waisraeli: ‘Chukueni mbuzi dume
kwa ajili ya sadaka ya dhambi, na ndama
na mwana-kondoo, wote wawili wawe wa
umri wa mwaka mmoja, na wasio na dosari,
kwa ajili ya sadaka ya kuteketezwa, 4 [d]na
pia maksai na kondoo dume kwa ajili ya
sadaka ya amani, ili kutoa dhabihu mbele
za BWANA, pamoja na sadaka ya nafaka
iliyochanganywa na mafuta. Kwa kuwa leo
BWANA atawatokea.’ ”

5 Wakavileta vile vitu Mose alivyowaagiza
mbele ya Hema la Kukutania, nalo
kusanyiko lote likakaribia na kusimama
mbele za BWANA. 6 Ndipo Mose akasema,
“Hili ndilo BWANA alilowaagiza mlifanye,
ili utukufu wa BWANA upate kuonekana
kwenu.”

7 [e]Mose akamwambia Aroni, “Njoo
madhabahuni ili utoe dhabihu yako ya
sadaka ya dhambi na sadaka yako ya
kuteketezwa, ufanye upatanisho kwa ajili
yako mwenyewe na kwa ajili ya watu.
Kisha utoe sadaka ya upatanisho kwa ajili
ya watu, kama vile BWANA alivyoagiza.”

8 [f]Hivyo Aroni akaja madhabahuni na
kumchinja yule ndama kuwa sadaka ya
dhambi kwa ajili yake mwenyewe. 9 Wanawe
wakamletea damu, naye akachovya kidole
chake katika hiyo damu, akaitia kwenye
pembe za madhabahu, nayo damu iliyobaki
akaimwaga chini ya madhabahu. 10 Juu ya
madhabahu akateketeza mafuta, figo na
mafuta yanayofunika ini kutoka kwenye
hiyo sadaka ya dhambi, kama BWANA
alivyomwagiza Mose. 11 [g]Akateketeza
nyama na ngozi nje ya kambi.

12 [h]Kisha Aroni akachinja sadaka ya
kuteketezwa. Wanawe wakamletea
damu, naye akainyunyiza pande zote za
madhabahu. 13 [i]Wakamletea sadaka ya
kuteketezwa kipande kwa kipande, pamoja
na kichwa, naye akaviteketeza juu ya
madhabahu. 14 [j]Akasafisha sehemu za ndani
na miguu, akaviteketeza juu ya sadaka ya
kuteketezwa juu ya madhabahu.

15 [k]Kisha Aroni akaleta sadaka ile
iliyokuwa kwa ajili ya watu. Akachukua
yule mbuzi wa sadaka ya dhambi kwa ajili
ya watu, akamchinja na kumtoa kwa ajili
ya sadaka ya dhambi, kama alivyofanya
kwa ile ya kwanza.

16 [l]Aroni akaleta sadaka ya kuteketezwa
na kuitoa kama ilivyoelekezwa. 17 [m]Pia
akaleta sadaka ya nafaka, akachukua konzi
moja na kuiteketeza juu ya madhabahu,
pamoja na sadaka ya kuteketezwa ya
asubuhi.

18 Akachinja maksai na kondoo dume
kama sadaka ya amani kwa ajili ya watu.
Wanawe Aroni wakampa ile damu, naye
akainyunyiza kwenye madhabahu pande
zote. 19 Lakini sehemu zile za mafuta ya
yule maksai na kondoo dume, yaani mafuta
ya mkia, mafuta yaliyofunika tumbo, ya
figo na yaliyofunika ini, 20 hivi vyote
wakaviweka juu ya vidari, kisha Aroni

---

[a]**9:1** Eze 43:27; Law 4:15
[b]**9:2** Law 4:3; 8:14-18
[c]**9:3** Law 4:3, 32; 10:16; Ezr 6:17; Isa 53:10; Rum 8:3; 1Pet 2:24
[d]**9:4** Law 4:10; Kut 32:6; 29:43; 9:6; 16:7; 24:16; 40:34-35; 1Fal 8:10-12
[e]**9:7** Law 16:6; Kut 30:10; Ebr 4:1-4; 7:27; 1Sam 3:14
[f]**9:8** Law 4:1-12; 10:19; 9:9; Kut 29:12; Eze 43:20; Law 4:7; 8:15
[g]**9:11** Law 4:11-12
[h]**9:12** Law 10:19
[i]**9:13** Law 1:8-9
[j]**9:14** Isa 53:10; 1Kor 15:3; 2Kor 5:21; Gal 1:4; Ebr 2:17; 1Pet 2:24; 3:18
[k]**9:15** Law 4:27-31
[l]**9:16** Law 1:1-13
[m]**9:17** Law 2:1-2; 3:5; Kut 29:38; 9:18; Law 3:1-11

akayateketeza hayo mafuta ya wanyama
juu ya madhabahu. 21 [a]Aroni akaviinua vile
vidari na paja la kulia mbele za BWANA
ili viwe sadaka ya kuinuliwa, kama Mose
alivyoagiza.
22 [b]Kisha Aroni akainua mikono yake
kuwaelekea watu na kuwabariki. Naye
baada ya kutoa dhabihu ya sadaka ya
dhambi, sadaka ya kuteketezwa, na sadaka
ya amani, akashuka chini.
23 [c]Kisha Mose na Aroni wakaingia
kwenye Hema la Kukutania. Walipotoka
nje, wakawabariki watu. Nao utukufu
wa BWANA ukawatokea watu wote.
24 [d]Moto ukaja kutoka uwepo wa BWANA,
ukairamba ile sadaka ya kuteketezwa,
pamoja na sehemu ya mafuta yaliyokuwa
juu ya madhabahu. Watu wote walipoona
jambo hili, wakapiga kelele kwa furaha na
kusujudu.

*Kifo Cha Nadabu Na Abihu*

10 [e]Nadabu na Abihu, wana wa Aroni,
wakachukua vyetezo vyao, wakaweka
moto ndani yake na kuongeza uvumba;
kisha wakamtolea BWANA moto usio halali,
kinyume na agizo la Mungu. 2 [f]Hivyo moto
ukaja kutoka kwa uwepo wa BWANA na
kuwaramba, nao wakafa mbele za BWANA.
3 [g]Kisha Mose akamwambia Aroni, "Hili
ndilo alilonena BWANA wakati aliposema:

" 'Miongoni mwa wale
watakaonikaribia
nitajionyesha kuwa mtakatifu;
machoni pa watu wote
nitaheshimiwa.' "

Aroni akanyamaza.
4 [h]Mose akawaita Mishaeli na Elisafani,
wana wa Uzieli mjomba wake Aroni,
akawaambia, "Njooni hapa. Ondoeni miili
ya binamu zenu mbele ya mahali patakatifu,
mkaipeleke nje ya kambi." 5 [i]Hivyo wakaja
na kuwaondoa, wakiwa bado wamevalia
makoti yao ya ibada, wakawapeleka nje ya
kambi, kama Mose alivyoamuru.
6 Ndipo Mose akamwambia Aroni pamoja
na wanawe, Eleazari na Ithamari, "Msifunue
vichwa vyenu wala msirarue mavazi yenu,
la sivyo mtakufa na BWANA ataikasirikia
jumuiya nzima. Lakini ndugu zenu, nyumba
yote ya Israeli, wanaweza kuwaombolezea
wale ambao BWANA amewaangamiza kwa
moto. 7 [j]Msitoke nje ya ingilio la Hema la
Kukutania, la sivyo mtakufa, kwa sababu
mafuta ya BWANA ya upako yako juu
yenu." Hivyo wakafanya kama vile Mose
alivyosema.
8 Kisha BWANA akamwambia Aroni,
9 [k]"Wewe na wanao msinywe mvinyo wala
kinywaji kingine kilichochachuka wakati
mwingiapo katika Hema la Kukutania,
la sivyo mtakufa. Hili litakuwa Agizo la
kudumu kwa vizazi vijavyo. 10 [l]Ni lazima
mtenganishe kilicho kitakatifu na kile
kilicho cha kawaida, kati ya yaliyo najisi
na yaliyo safi, 11 na lazima mwafundishe
Waisraeli amri zote ambazo BWANA aliwapa
kupitia Mose."

---

[a]**9:21** Kut 29:24-26; Law 7:30-34
[b]**9:22** Mwa 48:20; Kut 39:43; Lk 24:50
[c]**9:23** Kut 40:2; 24:16; 2Sam 6:18; 2Nya 16:2; Hes 16:19
[d]**9:24** Kut 19:18; Amu 6:21; 13:20; 1Fal 18:39; Mwa 15:17; 2Nya 7:1; Ezr 3:1
[e]**10:1** Kut 6:23; 24:1; 28:1; 30:9; Hes 3:2-4; 16:46; 26:61; 16:7, 18; 1Nya 6:3; 1Fal 7:50; Yer 52:19; 2Fal 25:15; 2Nya 4:22; Eze 8:11; Law 16:12; Isa 6:6
[f]**10:2** Za 2:12; 50:3; 106:18; Hes 11:1; 16:35; Isa 29:6; Mwa 19:24; 38:7; 1Nya 24:2; Ay 1:16
[g]**10:3** Kut 14:4; 19:22; 30:29; Law 21:6; 22:32; Hes 16:5; 20:13; Isa 5:16; 44:23; 49:3; 55:5; 60:21; Eze 28:22; 38:16
[h]**10:4** Kut 6:18-22; 25:8; Mdo 5:6-10
[i]**10:5** Law 8:13; 10:6; Kut 6:23; Law 13:45; 21:10; Hes 1:53; 5:18; 16:22; 20:29; Yer 41:5; Mk 14:63; Yos 7:1; 22:18; Mwa 50:3, 10; 1Sam 25:1
[j]**10:7** Kut 25:8; 28:41; Law 21:12
[k]**10:9** Mwa 9:21; Kut 12:14; 29:40; Law 23:13; Hes 6:3; 15:5; 28:7; Kum 14:26; 28:39; 29:6; Isa 5:22; 22:13; 28:1, 7; Yer 35:6; Hos 4:11; Hab 2:15-16; Amu 13:4; Mit 21:1; 23:29-35; 31:4-7; Eze 44:21; Mik 2:11; Lk 1:15; Efe 5:18; 1Tim 3:3; Tit 1:7
[l]**10:10** Mwa 7:2; Law 6:27; 14:57; 20:25; Eze 22:26; 10:11; 2Nya 15:3; 17:7; Ezr 7:25; Neh 8:7; Mal 2:7; Kum 17:10-11; 24:8; 25:1; 33:10; Mit 4:27; Hag 2:11

[12] [a]Mose akamwambia Aroni pamoja na wanawe waliosalia, Eleazari na Ithamari, "Chukueni sadaka ya nafaka iliyobaki kutoka sadaka zilizotolewa kwa BWANA kwa moto, muile hapo kando ya madhabahu ikiwa imeandaliwa bila chachu, kwa sababu ni takatifu sana. [13] Mtaila katika mahali patakatifu kwa sababu ni fungu lenu na fungu la wana wenu la sadaka zilizotolewa kwa BWANA kwa moto, kwa maana hivyo ndivyo nilivyoamriwa. [14] [b]Lakini wewe na wanao na binti zako mwaweza kula kidari kile kilichoinuliwa na paja lile lililotolewa. Mtavila mahali safi pa kawaida ya ibada; mmepewa wewe na watoto wako kuwa fungu lenu la sadaka za amani za Waisraeli. [15] [c]Paja lile lililotolewa na kidari kile kilichoinuliwa lazima viletwe pamoja na sehemu za mafuta ya sadaka za kuteketezwa kwa moto, ili kuinuliwa mbele za BWANA kama sadaka ya kuinuliwa. Hili litakuwa fungu lako la kawaida na wanao, kama BWANA alivyoagiza."

[16] [d]Mose alipouliza kuhusu mbuzi atolewaye kwa ajili ya sadaka ya dhambi, na kukuta kwamba ameteketezwa, aliwakasirikia Eleazari na Ithamari, wana wa Aroni waliobaki, akawauliza, [17] [e]"Kwa nini hamkula sadaka ya dhambi katika eneo la mahali patakatifu? Ni takatifu sana. Mlipewa ninyi ili kuondoa hatia ya jumuiya kwa ajili ya kuwafanyia upatanisho mbele za BWANA. [18] [f]Kwa kuwa damu yake haikuletwa ndani ya Mahali Patakatifu, mngemla mbuzi huyo katika sehemu ya mahali patakatifu kama nilivyoagiza."

[19] [g]Aroni akamjibu Mose, "Leo wanangu wametoa sadaka zao za dhambi na sadaka zao za kuteketezwa mbele za BWANA, lakini mambo kama haya yamenitokea mimi. Je, BWANA angependezwa kama ningekuwa nimekula sadaka ya dhambi leo?" [20] Mose aliposikia haya, akaridhika.

*Vyakula Najisi Na Visivyo Najisi*

**(Kumbukumbu 14:3-21)**

11 BWANA akawaambia Mose na Aroni, [2] [h]"Waambieni Waisraeli: 'Kati ya wanyama wote waishio juu ya nchi, hawa ndio mtakaowala: [3] Mwaweza kula mnyama yeyote mwenye kwato zilizogawanyika sehemu mbili na ambaye hucheua.

[4] " 'Kuna wanyama wengine ambao hucheua tu au wenye kwato zilizogawanyika tu, lakini hao kamwe msiwale. Ngamia ingawa hucheua hana kwato zilizogawanyika; kwa kawaida ya ibada hiyo ni najisi kwenu. [5] Pelele ingawa hucheua hana kwato zilizogawanyika; huyo ni najisi kwenu. [6] [i]Sungura ingawa hucheua hana kwato zilizogawanyika; huyo ni najisi kwenu. [7] [j]Naye nguruwe ingawa anazo kwato zilizogawanyika sehemu mbili, hacheui; huyo ni najisi kwenu. [8] [k]Kamwe msile nyama yao wala kugusa mizoga yao; wao ni najisi kwenu.

[9] " 'Kuhusu viumbe wote wanaoishi ndani ya maji ya bahari na vijito, mtakula wale wote wenye mapezi na magamba. [10] [l]Lakini viumbe wote ndani ya bahari au vijito wasio na mapezi na magamba, wakiwa miongoni mwa makundi au viumbe wote ndani ya maji, hao ni machukizo kwenu. [11] [m]Nao watakuwa machukizo kwenu. Msile nyama yao, nayo mizoga yao itakuwa machukizo. [12] Chochote kinachoishi ndani ya maji ambacho hakina mapezi na magamba kitakuwa chukizo kwenu.

[13] [n]" 'Wafuatao ndio ndege watakaokuwa machukizo kwenu, hivyo msiwale kwa sababu ni chukizo: tai, furukombe, kipungu,

---

[a]**10:12** Kut 29:41; Law 6:14-18; 10:13; 6:16; Eze 42:13
[b]**10:14** Hes 5:9; Kut 29:31; Law 4:12
[c]**10:15** Law 7:34; Kut 29:28
[d]**10:16** Law 9:3
[e]**10:17** Law 6:24-30; Eze 42:13; Kut 28:38
[f]**10:18** Law 4:18; 6:17, 26, 30
[g]**10:19** Law 9:12; Yer 6:20; 14:12; Hos 9:4; Mal 1:10
[h]**11:2** Mdo 10:12-14; Kum 14:4; Eze 4:4; Mt 15:11; Rum 14:2; 1Kor 8:8; Kol 2:16; Ebr 9:10
[i]**11:6** 1Tim 4:4-5
[j]**11:7** Isa 65:4; 66:3, 17
[k]**11:8** Isa 52:11; Law 5:2; Ebr 9:10; Mt 15:11, 20; Mdo 10:14-15; 15:29; Rum 14:14-17; 1Kor 8:8
[l]**11:10** Law 7:18; Kum 14:3
[m]**11:11** Law 5:2
[n]**11:13** Kum 14:12; Rum 14:1-23

14 [a]mwewe mwekundu, aina zote za mwewe
mweusi, 15 [b]aina zote za kunguru, 16 mbuni,
kiruka-njia, dudumizi, kipanga, shakwe,
aina zote za kipanga, 17 bundi, mnandi,
bundi mkubwa, 18 [c]mumbi, mwari, nderi,
19 [d]korongo, koikoi wa aina yoyote,
hudihudi na popo.

20 [e]“ ‘Wadudu wote warukao ambao
hutembea kwa miguu minne watakuwa
chukizo kwenu. 21 Lakini wako viumbe
wenye mabawa ambao hutembea kwa
miguu minne mtakaowala: wale wenye
vifundo katika miguu yao ya kurukaruka
juu ya ardhi. 22 Miongoni mwa hawa,
mtakula nzige wa aina zote, senene, parare
au panzi. 23 Lakini viumbe wengine wote
wenye mabawa na wenye miguu minne ni
machukizo kwenu.

*Wanyama Ambao Ni Najisi*

24 [f]“ ‘Mtajinajisi kwa wanyama hawa.
Yeyote agusaye mizoga yao atakuwa najisi
mpaka jioni. 25 [g]Yeyote atakayebeba mizoga
ya viumbe hawa ni lazima afue nguo zake,
naye atakuwa najisi mpaka jioni.

26 “ ‘Kila mnyama mwenye ukwato
ulioachana lakini haukugawanyika kabisa,
au yule asiyecheua, huyo ni najisi kwenu;
yeyote agusaye mzoga wowote wa hao
atakuwa najisi. 27 Miongoni mwa wanyama
wote watembeao kwa miguu minne, wale
watembeao kwa vitanga vyao ni najisi
kwenu; yeyote agusaye mizoga yao atakuwa
najisi mpaka jioni. 28 [h]Yeyote atakayebeba
mizoga yao ni lazima afue nguo zake, naye
atakuwa najisi mpaka jioni. Wanyama hawa
ni najisi kwenu.

29 “ ‘Kuhusu wanyama watambaao juu
ya ardhi, hawa ni najisi kwenu: kicheche,
panya, aina yoyote ya mijusi mikubwa,
30 [i]guruguru, kenge, mijusi ya ukutani,
goromoe na kinyonga. 31 Hao wote
watambaao juu ya ardhi ni najisi kwenu.
Yeyote agusaye mizoga yao atakuwa najisi
mpaka jioni. 32 [j]Ikiwa mmoja wao atakufa
na kuangukia juu ya kitu fulani, chombo
hicho, hata kikiwa cha matumizi gani,
kitakuwa najisi, kiwe kimetengenezwa
kwa mti, nguo, ngozi au gunia. Kiweke
ndani ya maji; kitakuwa najisi mpaka
jioni, kisha kitakuwa safi tena. 33 [k]Ikiwa
mmoja wa wanyama aliyekufa ataangukia
ndani ya chungu, kila kilichomo katika
chungu hicho kitakuwa najisi, nawe ni
lazima uvunje chungu hicho. 34 Chakula
chochote ambacho chaweza kuliwa lakini
kikawa kimeingia maji kutoka kwenye
chungu hicho ni najisi, na kitu chochote
cha majimaji ambacho chaweza kunyweka
kutoka kwenye chungu hicho ni najisi.
35 Chochote ambacho mzoga wa mmojawapo
utaangukia kitakuwa najisi. Jiko au chungu
cha kupikia ni lazima kivunjwe. Ni najisi,
nawe ni lazima uvihesabu kuwa najisi.
36 Lakini chemchemi au kisima, mahali pa
kuchota maji, patakuwa safi, lakini yeyote
atakayegusa moja ya mizoga hii ni najisi.
37 Kama mzoga ukianguka juu ya mbegu
zozote ambazo ni za kupanda, zinabaki
safi. 38 Lakini kama mbegu imetiwa maji
na mzoga ukaanguka juu yake, hiyo mbegu
ni najisi kwenu.

39 [l]“ ‘Kama mnyama ambaye mnaruhusiwa
kumla akifa, yeyote atakayeugusa mzoga
wake atakuwa najisi mpaka jioni. 40 [m]Yeyote
atakayekula sehemu ya mzoga huo ni
lazima afue nguo zake, naye atakuwa najisi
mpaka jioni. Yeyote atakayebeba mzoga
huo ni lazima afue nguo zake, naye atakuwa
najisi mpaka jioni.

41 “ ‘Kila kiumbe kitambaacho juu ya
ardhi ni chukizo; kisiliwe. 42 Msile kiumbe

---

[a]**11:14** Mwa 1:11
[b]**11:15** Mwa 8:7
[c]**11:18** Isa 13:21; 14:23; 34:11-14; Sef 2:14
[d]**11:19** Zek 5:9; Mwa 1:11; Isa 2:20
[e]**11:20** Mdo 10:14; 11:22; Mt 3:4; Mk 1:6
[f]**11:24** Law 5:2; 13:3; 14:46; 15:5; 22:6; Hes 19:7, 19; Amu 6:5; Yer 46:23; Nah 3:17
[g]**11:25** Kut 19:10; Law 13:6, 34; 14:8; 15:5; 16:26; Hes 8:7; 19:7-8; 31:24
[h]**11:28** Ebr 9:10; 11:29; Isa 66:17; Ebr 9:10; Isa 66:17
[i]**11:30** Za 58:8; Isa 2:20
[j]**11:32** Law 15:12; Hes 19:18; 31:20
[k]**11:33** Law 6:28; 15:12
[l]**11:39** Law 17:15; 22:4, 8; Kum 14:21; Eze 4:14; 44:31; Hes 19:11
[m]**11:40** Law 14:8; 17:15; 22:8; Eze 44:31; Ebr 9:10

chochote kitambaacho juu ya ardhi,
kiwe kitambaacho kwa tumbo lake, au
kitambaacho kwa miguu minne au kwa
miguu mingi; ni chukizo. 43 [a]Msijitie unajisi
kwa chochote katika viumbe hivi. Msijitie
unajisi kwa viumbe hivyo au kutiwa
unajisi navyo. 44 [b]Mimi ndimi BWANA
Mungu wenu; jitakaseni mwe watakatifu,
kwa sababu mimi ni mtakatifu. Msijitie
unajisi wenyewe kwa kiumbe chochote
kile kiendacho juu ya ardhi. 45 [c]Mimi ndimi
BWANA niliyewapandisha mtoke Misri
ili niwe Mungu wenu. Kwa hiyo kuweni
watakatifu kwa sababu Mimi ni mtakatifu.
46 " 'Haya ndiyo masharti kuhusu
wanyama, ndege, kila kiumbe hai kiendacho
ndani ya maji, na kila kiumbe kiendacho
juu ya ardhi. 47 [d]Ni lazima mpambanue
kati ya kilicho najisi na kilicho safi, kati
ya viumbe hai vinavyoweza kuliwa na vile
visivyoweza kuliwa.' "

*Utakaso Baada Ya Kuzaa Mtoto*

12 BWANA akamwambia Mose,
2 [e]"Waambie Waisraeli: 'Mwanamke
ambaye atapata mimba na kuzaa mtoto
wa kiume atakuwa najisi kwa kawaida ya
ibada kwa siku saba, kama anavyokuwa
najisi wakati wa siku zake za hedhi.
3 [f]Mvulana atatahiriwa siku ya nane. 4 Kisha
ni lazima huyo mwanamke asubiri kwa siku
thelathini na tatu, ndipo atakaswe kutoka
damu kwake. Hataruhusiwa kugusa kitu
chochote kilicho kitakatifu au kuingia
mahali patakatifu, mpaka siku za kutakaswa
kwake zimetimia. 5 Kama akimzaa mtoto
wa kike, mwanamke huyo atakuwa najisi
kwa majuma mawili, kama wakati wake
wa hedhi. Kisha atasubiri kwa siku sitini na
sita, ndipo atatakaswa kutoka damu kwake.
6 [g]" 'Siku zake za utakaso kwa ajili ya
mwana au binti zitakapotimia, mwanamke
huyo atamletea kuhani kwenye ingilio la
Hema la Kukutania mwana-kondoo mwenye
umri wa mwaka mmoja kwa ajili ya sadaka
ya kuteketezwa, na kinda la njiwa au hua
kwa ajili ya sadaka ya dhambi. 7 [h]Atavitoa
mbele za BWANA ili kufanya upatanisho
kwa ajili yake, na kisha atakuwa safi kwa
desturi ya ibada kutokana na kutokwa
damu kwake.
" 'Haya ndiyo masharti kwa ajili ya
mwanamke atakayezaa mtoto wa kiume
au wa kike. 8 [i]Kama huyo mwanamke hana
uwezo wa kumpata mwana-kondoo, ataleta
hua wawili au makinda mawili ya njiwa,
moja kwa ajili ya sadaka ya kuteketezwa na
mwingine kwa ajili ya sadaka ya dhambi.
Kwa njia hii, kuhani atafanya upatanisho
kwa ajili yake, naye atakuwa safi.' "

*Masharti Kuhusu Magonjwa Ya Ngozi Yaambukizayo*

13 BWANA akawaambia Mose na Aroni,
2 [j]"Iwapo mtu yeyote atakuwa na
uvimbe au upele au alama nyeupe juu ya
ngozi yake ambayo yaweza kuwa ugonjwa
wa ngozi wa kuambukiza,[k] ni lazima aletwe
kwa Aroni kuhani ama kwa wanawe,
kuhani mmojawapo. 3 [l]Kuhani atachunguza
hicho kidonda kilichopo juu ya ngozi
yake, na kama nywele za mahali palipo
na kidonda zimebadilika kuwa nyeupe, na
ikiwa kidonda kimeingia ndani ya ngozi,

[a]**11:43** Law 20:5; 22:5
[b]**11:44** Kut 6:2, 7; 19:10; 20:2; 22:31; 31:13; Isa 43:3; 51:15; Eze 20:5; Law 19:2; 20:7; Hes 15:40; Yos 3:5; 7:13; 24:19; 1Nya 15:12; 2Nya 29:5; 35:6; Kum 14:2; 1Sam 2:2; Ay 6:10; Za 99:3; Efe 1:4; 1The 4:7; 1Pet 1:15-16
[c]**11:45** Law 25:38, 55; Mwa 17:7; Kut 6:7; 19:6; 1Pet 1:16; Rum 14:17; 1Kor 6:11
[d]**11:47** Law 10:10; Yer 15:19; Eze 22:26; 44:23
[e]**12:2** Law 15:19; 18:19; Isa 64:6; Eze 18:6; 22:10; 36:17
[f]**12:3** Kut 22:30; Mwa 17:10-12; Lk 1:59; 2:21; 2:2; Yn 7:22-23
[g]**12:6** Lk 2:22; Kut 29:38; Law 5:7; 23:12; Hes 6:12-14; 7:15; Ufu 5:6-8; 7:14
[h]**12:7** Ebr 9:9-28; 10:1-12
[i]**12:8** Mwa 15:9; Law 4:26; 14:22; 5:7; Lk 2:22-24; Law 4:26; 2Kor 8:9
[j]**13:2** Law 14:3, 32, 56; Kut 4:6; Hes 5:2; Kum 24:8; 28:27; Isa 3:17; Eze 22:26; Mt 8:2-4; 10:8; Lk 17:1-16; Yn 13:8-10
[k]2 Ugonjwa wa ngozi wa kuambukiza, yaani ukoma, ni neno lililotumika kwa Kiebrania kueleza magonjwa mbalimbali ya ngozi ambayo si lazima yawe ni ukoma halisi.
[l]**13:3** Law 21:1; Hes 9:6; 13:4; Law 14:38; Hes 12:14-15; Kum 24:9

basi ni ugonjwa wa ngozi wa kuambukiza,
yaani ukoma. Kuhani atakapomchunguza,
atamtangaza mtu huyo kuwa ni najisi kwa
kawaida ya ibada. 4 Kama alama juu ya
ngozi yake ni nyeupe, lakini haionekani
kuwa imeingia ndani zaidi ya ngozi, na
nywele kwenye alama hiyo hazijageuka
kuwa nyeupe, kuhani atamtenga mtu huyo
mahali pa pekee kwa siku saba. 5 [a]Siku
ya saba, kuhani atamchunguza, na kama
hakuona badiliko kwenye kile kidonda na
hakijaenea juu ya ngozi, atamtenga kwa
siku nyingine saba. 6 [b]Siku ya saba kuhani
atamchunguza tena, na kama kidonda
kimepungua na hakijaenea juu ya ngozi,
kuhani atamtangaza mtu huyo kuwa ni
safi, ni upele tu. Ni lazima mtu huyo afue
mavazi yake, naye atakuwa safi. 7 [c]Lakini
ikiwa ule upele utaenea juu ya ngozi yake
baada ya yeye kujionyesha kwa kuhani na
kutangazwa kuwa safi, ni lazima aende
tena kwa kuhani. 8 Kuhani atamchunguza,
na kama upele umeenea kwenye ngozi,
atamtangaza kuwa najisi, kwani ni ugonjwa
wa ngozi wa kuambukiza, yaani ukoma.

9 “Wakati mtu yeyote ana ugonjwa wa
ngozi wa kuambukiza, ni lazima aletwe
kwa kuhani. 10 [d]Kuhani atamchunguza na
kama kuna uvimbe mweupe juu ya ngozi
ambao umefanya nywele kuwa nyeupe, na
kama kuna nyama mbichi ndani ya uvimbe,
11 [e]ni ugonjwa sugu wa ngozi, na kuhani
atamtangaza kuwa najisi. Hatamtenga tena
kwa sababu ni najisi tayari.

12 “Ikiwa ugonjwa utakuwa umeenea
kwenye ngozi yake yote kwa kadiri kuhani
atakavyoweza kuona, kwamba umeenea
kwenye ngozi yote ya huyo mgonjwa
kutoka kichwani mpaka wayo, 13 kuhani
atamchunguza, na kama ugonjwa umeenea
mwili mzima, atamtangaza huyo mtu kuwa
safi. Kwa kuwa mwili wote umekuwa
mweupe, yeye ni safi. 14 [f]Lakini itokeapo
nyama mbichi kwenye ngozi yake, atakuwa
najisi. 15 [g]Kuhani atakapoiona hiyo nyama
mbichi, atamtangaza mtu huyo kuwa
najisi. Hiyo nyama mbichi ni najisi, ana
ugonjwa wa kuambukiza. 16 Hiyo nyama
mbichi ikigeuka na kuwa nyeupe, ni
lazima amwendee kuhani. 17 Kuhani
atamchunguza, na kama vidonda vimekuwa
vyeupe, kuhani atamtangaza mgonjwa huyo
kuwa safi; kisha atakuwa safi.

18 [h]“Wakati mtu ana jipu juu ya ngozi yake
nalo likapona, 19 napo mahali palipokuwa
na jipu pakatokea uvimbe mweupe, au
alama yenye wekundu na weupe, ni
lazima akajionyeshe kwa kuhani. 20 Kuhani
atapachunguza, na kama uvimbe umezama
ndani ya ngozi, na nywele zimegeuka
kuwa nyeupe, kuhani atamtangaza mtu
huyo kuwa najisi. Ni ugonjwa wa ngozi
wa kuambukiza uliojitokeza pale jipu
lilipokuwa. 21 Lakini ikiwa wakati kuhani
anapopachunguza pakawa hapana nywele
nyeupe ndani yake, wala hakuna shimo
bali pamepungua, basi kuhani atamtenga
mtu huyo kwa siku saba. 22 Kama unaenea
kwenye ngozi, kuhani atamtangaza kuwa
najisi; ni ugonjwa wa ngozi wa kuambukiza.
23 [i]Lakini ikiwa ile alama haijabadilika wala
kuenea, ni kovu tu kutokana na jipu, kuhani
atamtangaza kuwa safi.

24 “Wakati mtu ameungua kwenye ngozi
yake, pakatokea alama yenye wekundu
na weupe, au alama nyeupe ikaonekana
penye nyama mbichi pale palipoungua,
25 kuhani ataichunguza ile alama, na kama
nywele zilizoko juu yake zimegeuka kuwa
nyeupe, napo pametokea shimo, basi huo ni
ugonjwa wa ngozi wa kuambukiza ambao
umetokea juu ya jeraha la moto. Kuhani
atamtangaza kuwa najisi; ni ugonjwa wa
ngozi wa kuambukiza. 26 Lakini kama kuhani
akichunguza na kuona kwamba hakuna
nywele nyeupe kwenye alama ile, wala
hakuna shimo napo pameanza kupungua,

[a]**13:5** Law 14:9
[b]**13:6** Mt 8:3; Lk 5:12-14; Law 11:25; 14:8, 9, 20; 15:8; Hes 8:7
[c]**13:7** Lk 5:14; 13:8
[d]**13:10** Mk 1:44; Lk 17:14; Hes 12:10; 2Nya 26:19-20
[e]**13:11** Kut 4:6; Law 14:8; Hes 12:10; Mt 8:2
[f]**13:14** Lk 5:12-14
[g]**13:15** Kum 32:29; Za 147:3
[h]**13:18** Kut 9:9; 15:26; Za 38:3-7; Isa 38:21; Kum 28:27; 2Fal 20:7; 13:19; Law 14:37
[i]**13:23** Mit 28:13; Lk 5:14; 1Pet 4:2-4

basi kuhani atamtenga kwa siku saba.
27 Siku ya saba kuhani atamchunguza tena,
na kama unaenea kwenye ngozi, kuhani
atamtangaza kuwa najisi; ni ugonjwa wa
ngozi wa kuambukiza. 28 [a]Lakini, kama
alama ile haikubadilika na wala haijaenea
kwenye ngozi, napo pamepungua, ni
uvimbe kutokana na jeraha la moto, na
kuhani atamtangaza kuwa safi; ni kovu tu
kutokana na kuungua.

29 “Ikiwa mwanaume au mwanamke ana
kidonda juu ya kichwa au juu ya kidevu,
30 kuhani atakichunguza kile kidonda,
na kama ataona kuwa kimeingia ndani,
na nywele zilizoko juu yake ni njano na
nyembamba, kuhani atamtangaza mtu huyo
kuwa najisi, kwani ni upele; ni ugonjwa
wa ngozi wa kuambukiza wa kichwa au
kidevu. 31 Lakini kama kuhani akichunguza
aina hii ya kidonda, kionekane kuwa
hakina shimo na hakuna nywele nyeusi juu
yake, basi atamtenga mtu huyo kwa siku
saba. 32 Siku ya saba kuhani atachunguza
kidonda kile, na kama upele haujaenea,
na hakuna nywele za manjano juu yake,
wala hakuna shimo lolote, 33 mtu huyo
ni lazima anyolewe, isipokuwa mahali
palipo na ugonjwa, naye kuhani atamtenga
kwa siku nyingine saba. 34 [b]Siku ya saba
kuhani atachunguza tena ule upele; ikiwa
haujaenea kwenye ngozi na hakuna shimo
mahali pale, kuhani atamtangaza kuwa
safi. Lazima afue nguo zake, naye atakuwa
safi. 35 Lakini ikiwa upele utaenea juu ya
ngozi baada ya kutangazwa kuwa safi,
36 kuhani atamchunguza, na kama upele
umeenea kwenye ngozi, kuhani hana
haja ya kutazama kama kuna nywele
za manjano, mtu huyo ni najisi. 37 Hata
hivyo, katika uchunguzi wake akiona
hapajabadilika, na nywele nyeusi zimeota
juu yake, upele umepona. Yeye si najisi,
kuhani atamtangaza kuwa safi.

38 “Ikiwa mwanaume au mwanamke
ana alama nyeupe juu ya ngozi yake,
39 kuhani atamchunguza, na kama alama
hizo zina weupe uliofifia, ni vipele visivyo
na madhara vilivyojitokeza kwenye ngozi;
mtu huyo ni safi.

40 [c]“Wakati mwanaume hana nywele naye
ana upaa, yeye ni safi. 41 Ikiwa hana nywele
kwenye ngozi ya kichwa chake, na ana upaa
tangu kwenye paji, ni safi. 42 Lakini kama ana
kidonda chenye wekundu na weupe kwenye
kichwa chake chenye upaa, au kwenye paji
la uso, ni ugonjwa wa ngozi wa kuambukiza
unaojitokeza kichwani au kwenye paji
lake la uso. 43 Kuhani atamchunguza, na
kama kidonda kilichovimba juu ya kichwa
chake au kwenye paji la uso ni chekundu
au cheupe kama ugonjwa wa ngozi wa
kuambukiza, 44 mtu huyo ni mgonjwa, na ni
najisi. Kuhani atamtangaza kuwa najisi kwa
sababu ya kidonda kwenye kichwa chake.

45 [d]“Mtu mwenye ugonjwa kama huo
wa kuambukiza ni lazima avae nguo
zilizoraruka, awachilie nywele zake bila
kuzichana, afunike sehemu ya chini ya
uso wake, na apige kelele, ‘Najisi! Najisi!’
46 [e]Kwa muda wote atakaokuwa na ugonjwa
huo wa kuambukiza atabaki kuwa najisi.
Ni lazima aishi peke yake; ni lazima aishi
nje ya kambi.

### *Masharti Kuhusu Upele*

47 “Kama vazi lolote lina maambukizo
ya upele: likiwa ni vazi la sufu au kitani,
48 lolote lililofumwa au kusokotwa likiwa
la kitani au la sufu, ngozi yoyote au
chochote kilichotengenezwa kwa ngozi,
49 tena kama maambukizo kwenye vazi,
au ngozi, au lililofumwa au kusokotwa,
au kifaa chochote cha ngozi, ni rangi ya
kijani au nyekundu, huo ni upele unaoenea
na ni lazima kuhani aonyeshwe. 50 Kuhani
atachunguza upele huo na kukitenga
kifaa hicho kwa siku saba. 51 [f]Siku ya saba
atakichunguza, na kama upele umeenea
kwenye nguo, au kifaa kilichofumwa au
kusokotwa, au ngozi, kwa vyovyote vile

---

[a]**13:28** Kum 24:8; Mal 2:7; 1Kor 12:9; Isa 3:17
[b]**13:34** Law 11:25
[c]**13:40** Law 21:5; 2Fal 2:23; Isa 3:24; 15:2; 22:12; Eze 27:31; 29:18; Amo 8:10; Mik 1:16
[d]**13:45** Law 5:2; 10:6; Eze 24:17, 22; Mik 3:7; Mao 4:15; Lk 17:12
[e]**13:46** Hes 5:1-4; 12:14; 2Fal 7:3; 15:5; 1Kor 5:5; 2The 3:6; Ebr 12:15
[f]**13:51** Law 14:44; Eze 16:42

itumikavyo, ni upele uangamizao, kifaa hicho ni najisi. [52] Ni lazima aichome hiyo nguo, ikiwa ni ya sufu ama kitani iliyofumwa ama kusokotwa, ama chombo chochote cha ngozi chenye maambukizo, kwa kuwa ni upele unaoangamiza; chombo chote ni lazima kichomwe moto.

[53] "Lakini wakati kuhani atakapokichunguza na kuona kuwa ule upele haujaenea kwenye nguo iliyofumwa au kusokotwa, au vifaa vya ngozi, [54] ataagiza kwamba kifaa chenye maambukizo kisafishwe. Kisha atakitenga kwa siku saba. [55] Baada ya kifaa chenye maambukizo kusafishwa, kuhani atakichunguza, na kama upele haujaonyesha badiliko lolote, hata kama haujaenea, ni najisi. Kichome kwa moto, iwe upele umeenea upande mmoja au mwingine. [56] Kama kuhani ataona kuwa ile alama imefifia baada ya kuoshwa, basi atararua sehemu iliyo ambukizwa ya nguo au ngozi au kifaa kilichofumwa au kusokotwa. [57] Lakini kama ikijitokeza tena kwenye nguo au kitu kilichofumwa au kusokotwa, ama kifaa cha ngozi, kwamba ule upele unaenea, chochote chenye upele ni lazima kichomwe kwa moto. [58] Nguo, au kitu kilichofumwa au kusokotwa, au kifaa chochote cha ngozi ambacho kimesafishwa na kuondolewa upele, ni lazima kioshwe tena, nacho kitakuwa safi."

[59] Haya ni masharti kuhusu maambukizo ya upele kwenye mavazi ya sufu au kitani, yaliyofumwa ama kusokotwa, ama kifaa chochote cha ngozi, kwa ajili ya kuvitangaza kuwa safi au najisi.

### *Kutakasa Kutoka Maambukizo Ya Magonjwa Ya Ngozi*

14 Bwana akamwambia Mose, [2] [a]"Haya ndiyo masharti yamhusuyo mtu mgonjwa wakati wa kufanyiwa ibada ya utakaso wakati aletwapo kwa kuhani: [3] Kuhani atakwenda kumchunguza nje ya kambi. Kama mtu huyo atakuwa amepona ugonjwa wake wa ngozi wa kuambukiza, [4] [b]kuhani ataagiza vitu vifuatavyo viletwe kwa ajili ya mtu atakayetakaswa: ndege wawili safi walio hai, mti wa mwerezi, kitani nyekundu, na hisopo. [5] Kisha kuhani ataagiza kwamba mmoja wa ndege wale achinjwe kwenye chungu chenye maji safi. [6] Kisha kuhani atamchukua ndege aliye hai na kumtumbukiza pamoja na mti wa mwerezi, kitani nyekundu na hisopo ndani ya damu ya yule ndege aliyechinjiwa kwenye maji safi. [7] [c]Atamnyunyizia yule mwenye ugonjwa wa kuambukiza maji hayo mara saba, na kumtangaza kuwa safi. Kisha atamwachia yule ndege aliye hai aende zake kwenye mashamba.

[8] [d]"Huyo mtu atakayetakaswa ni lazima afue nguo zake, anyoe nywele zake zote, na aoge kwa maji; ndipo atakapokuwa safi kwa desturi ya ibada. Baada ya hili anaweza kuingia kambini, lakini ni lazima akae nje ya hema lake kwa siku saba. [9] [e]Siku ya saba ni lazima anyoe nywele zake zote; yaani anyoe nywele za kichwa, ndevu zake, kope zake na nywele nyingine zote. Ni lazima afue nguo zake, na aoge kwa maji, naye atakuwa safi.

[10] [f]"Siku ya nane, ni lazima alete kondoo dume wawili na kondoo jike mmoja, wote wa mwaka mmoja na wasio na dosari, pamoja na sehemu tatu za kumi za efa[g] za unga laini uliochanganywa na mafuta, kwa ajili ya sadaka ya nafaka, na logi moja[h] ya mafuta. [11] [i]Kuhani atakayemtangaza kuwa safi atahitaji kumkabidhi mgonjwa aliyepona pamoja na sadaka zake zote mbele za Bwana katika ingilio la Hema la Kukutania.

[12] [j]"Kisha kuhani atamchukua mmoja wa

---

[a]**14:2** Law 13:57; Kum 24:8; Mt 8:2-4; Mk 1:40-44; Lk 5:12-14; 17:14
[b]**14:4** Kut 12:22; Hes 19:6; Za 51:7; Ebr 9:19
[c]**14:7** 2Fal 5:10-14; Isa 52:15; Eze 36:25; Law 8:11; Ebr 10:22
[d]**14:8** Law 11:25; 13:11; 15:5; 17:15; 22:6; Kut 29:4; Hes 5:2-3; 12:14-15; 19:7-8; 20; 31:24; 2Nya 26:21
[e]**14:9** Law 13:5-6; Hes 6:9; Kum 21:12
[f]**14:10** Hes 6:10; 15:9; 28:20; Mt 8:4; Mk 1:44; Lk 5:14; Law 2:1; 4:32
[g]10 Sehemu tatu za kumi za efa ni sawa na kilo 3.
[h]10 Logi ni kipimo cha ujazo ambacho ni sawa na lita 0.3.
[i]**14:11** Hes 6:10, 16
[j]**14:12** Law 5:18; 6:6-7; Kut 29:24

wale kondoo dume na kumtoa kuwa sadaka
ya hatia, pamoja na ile logi moja ya mafuta;
ataviinua mbele za BWANA kuwa sadaka
ya kuinuliwa. 13 [a]Atamchinja huyo kondoo
katika mahali patakatifu ambapo sadaka ya
dhambi na ile ya kuteketezwa huchinjiwa.
Kama ilivyo sadaka ya dhambi, sadaka ya
hatia ni ya kuhani; nayo ni takatifu sana.
14 [b]Kuhani atachukua sehemu ya damu ya
sadaka ya hatia na kuitia kwenye ncha ya
sikio la kuume la yule atakayetakaswa,
kwenye kidole gumba cha mkono wake wa
kuume, na kidole kikubwa cha mguu wake
wa kuume. 15 Kuhani atachukua sehemu
ya ile logi ya mafuta, ayamimine kwenye
kiganja cha mkono wake mwenyewe wa
kushoto, 16 na achovye kidole chake cha
shahada cha mkono wake wa kuume kwenye
mafuta yaliyoko kwenye kiganja chake, na
kwa kidole hicho anyunyize mafuta hayo
mara saba mbele za BWANA. 17 [c]Kuhani
atampaka yule anayetakaswa sehemu ya
mafuta yaliyobaki kiganjani kwenye ncha ya
sikio lake la kuume, kwenye kidole gumba
cha mkono wake wa kuume, na kidole
kikubwa cha mguu wake wa kuume, mahali
palepale alipompaka damu ya sadaka ya
kuondoa hatia. 18 [d]Kuhani atayapaka mafuta
yaliyobaki kwenye kiganja chake juu ya
kichwa cha yule anayetakaswa, na kufanya
upatanisho kwa ajili yake mbele za BWANA.

19 [e]"Kisha kuhani atatoa dhabihu ya
sadaka ya dhambi na kufanya upatanisho
kwa ajili ya yule atakayetakaswa kutoka
unajisi wake. Baada ya hayo, kuhani
atachinja sadaka ya kuteketezwa 20 [f]na
kuitoa juu ya madhabahu, pamoja na
sadaka ya nafaka ili kumfanyia upatanisho,
naye atakuwa safi.

21 [g]"Hata hivyo, kama ni maskini na
hawezi kupata vitu hivi, lazima achukue
mwana-kondoo mmoja kama sadaka
ya hatia ipate kuinuliwa ili kumfanyia
upatanisho, pamoja na sehemu ya kumi
ya efa[h] ya unga laini uliochanganywa na
logi moja ya mafuta kwa ajili ya sadaka ya
nafaka, 22 [i]na hua wawili au makinda mawili
ya njiwa, kile atakachoweza kupata, mmoja
kwa sadaka ya dhambi, na mwingine kwa
sadaka ya kuteketezwa.

23 "Katika siku ya nane, lazima avilete
vitu hivyo kwa kuhani, kwa ajili ya
kutakaswa kwake kwenye ingilio la Hema
la Kukutania mbele za BWANA. 24 [j]Kuhani
atamchukua mwana-kondoo kwa ajili ya
sadaka ya hatia, pamoja na ile logi ya
mafuta ya kuinuliwa mbele za BWANA
kuwa sadaka ya kuinuliwa. 25 [k]Atamchinja
huyo mwana-kondoo kwa ajili ya sadaka ya
hatia. Pia ataichukua sehemu ya damu yake
na kuipaka kwenye ncha ya sikio la kuume
la yule anayetakaswa, na aipake pia kwenye
kidole gumba cha mkono wa kuume wa
huyo mtu, na kidole kikubwa cha mguu
wake wa kuume. 26 Kuhani atamiminia
sehemu ya mafuta kwenye kiganja chake
cha mkono wa kushoto, 27 na kwa kidole
chake cha shahada cha mkono wa kuume,
atamnyunyizia yule anayetakaswa yale
mafuta yaliyo kwenye kiganja chake mara
saba mbele za BWANA. 28 Atampaka mafuta
yaliyobaki kwenye kiganja chake katika
sehemu zote, kama alivyompaka damu
ya sadaka ya hatia: yaani, kwenye ncha
ya sikio la kuume la yule anayetakaswa,
kwenye kidole gumba cha mkono wake
wa kuume, na kidole kikubwa cha mguu
wake wa kuume. 29 Kuhani atayapaka
mafuta yaliyobaki katika kiganja chake
kwenye kichwa cha yule anayetakaswa, na
kufanya upatanisho kwa ajili yake mbele
za BWANA. 30 [l]Kisha atatoa dhabihu wale

[a]**14:13** Kut 29:11; Law 6:24-30; 7:7; Isa 53:7; Yn 1:29; 1Pet 1:19; Ufu 5:6
[b]**14:14** Kut 29:20; Law 8:23; Ufu 12:11; Ebr 9:9-14; Kol 1:14; 2Kor 7:1
[c]**14:17** Rum 6:13-22; 1Kor 6:20
[d]**14:18** Law 15:15; 4:26; Hes 15:28; Dan 9:24; Rum 3:23-25; 5:11; Efe 2:12-22; Kol 1:19-22
[e]**14:19** Law 5:3; 15:15
[f]**14:20** Law 15:30
[g]**14:21** Law 5:7; 12:8; Ay 34:19; Mt 11:30; Lk 6:20; Mit 17:5; 1Yn 5:3
[h]21 Sehemu ya kumi ya efa ni sawa na lita 2.
[i]**14:22** Law 5:7; 15:30; 12:8; Lk 2:24
[j]**14:24** Hes 6:14; 1The 5:23; 1Yn 1:7; Ufu 7:14
[k]**14:25** Kut 29:20
[l]**14:30** Rum 8:3

hua ama yale makinda ya njiwa ambayo
mtu ataweza kuwapata, 31 [a]mmoja kwa ajili
ya sadaka ya dhambi, na mwingine kuwa
sadaka ya kuteketezwa, pamoja na sadaka
ya nafaka. Kwa njia hii kuhani atafanya
upatanisho mbele za BWANA kwa ajili ya
yule anayetakaswa."
32 [b]Haya ndiyo masharti kwa mtu yeyote
mwenye ugonjwa wa ngozi wa kuambukiza,
na ambaye hana uwezo wa kutoa sadaka
za kawaida kwa ajili ya kutakaswa kwake.

*Kutakaswa Upele*

33 BWANA akawaambia Mose na Aroni,
34 "Mtakapoingia katika nchi ya Kanaani
ambayo ninawapa kuwa milki yenu, nami
nikaweka upele ueneao kwenye nyumba
katika nchi ile, 35 [c]ni lazima mwenye nyumba
hiyo akamwambie kuhani, 'Nimeona kitu
fulani kinachofanana na upele kwenye
nyumba yangu.' 36 [d]Kuhani ataagiza vitu
vyote vitolewe ndani ya nyumba, kabla
hajaenda kuchunguza kama ina ugonjwa
huo, ili kitu chochote ndani ya nyumba
kisitangazwe kuwa najisi. Baada ya hili,
kuhani ataingia ndani na kuikagua hiyo
nyumba. 37 [e]Atachunguza upele huo katika
kuta za nyumba hiyo, nazo kama zina
rangi ya kijani kibichi au wekundu, na
kuna mibonyeo ndani ya ukuta, 38 kuhani
atatoka na kufunga mlango wa nyumba
hiyo kwa siku saba. 39 Siku ya saba, kuhani
atarudi kuikagua nyumba. Kama upele
umeenea juu ya kuta, 40 ataagiza kwamba
mawe yote yaliyoambukizwa yaondolewe
na kutupwa katika eneo lililo najisi nje ya
mji. 41 Kuta zote za ndani ya nyumba hiyo
ni lazima zikwanguliwe, na kifusi chake
kitupwe mahali najisi nje ya mji. 42 Kisha
watachukua mawe mengine na kujenga
palipobomolewa kwa udongo mpya wa
mfinyanzi, na kuipiga nyumba hiyo lipu
mpya.
43 "Ikiwa upele huo utatokea tena ndani
ya ile nyumba baada ya mawe kuondolewa
na nyumba kukwanguliwa na kuwekwa lipu
mpya, 44 [f]kuhani atakwenda kuikagua, na
kama upele umeenea ndani ya nyumba, basi
ni upele uharibuo; nyumba hiyo ni najisi.
45 Ni lazima ibomolewe: mawe yake, mbao
na lipu yake, vyote vikatupwe nje ya mji
mahali palipo najisi.
46 [g]"Yeyote atakayeingia katika nyumba
hiyo ikiwa imefungwa, atakuwa najisi
mpaka jioni. 47 [h]Yeyote atakayelala au kula
ndani ya nyumba hiyo ni lazima afue nguo
zake.
48 [i]"Lakini ikiwa kuhani atakuja kuikagua
na kukuta kuwa upele haujaenea tena
baada ya nyumba kupigwa lipu, ataitangaza
nyumba ile kuwa safi, kwa sababu upele
umekwisha. 49 [j]Ili kuitakasa nyumba hiyo,
mwenye nyumba ataleta ndege wawili, mti
wa mwerezi, kitani nyekundu na hisopo.
50 Atamchinja mmoja wa wale ndege kwenye
chungu chenye maji safi. 51 [k]Kisha atachukua
mti wa mwerezi, hisopo, kitani nyekundu
na ndege aliye hai, na kuvitumbukiza ndani
ya damu ya ndege aliyechinjwa pamoja na
maji safi, na kuinyunyizia nyumba ile mara
saba. 52 Ataitakasa nyumba kwa damu ya
yule ndege, maji safi, ndege aliye hai, mti
wa mwerezi, hisopo na kitani nyekundu.
53 Kisha atamwachia yule ndege aliye hai
huru mashambani nje ya mji. Kwa njia hii
atafanya upatanisho kwa ajili ya nyumba
ile, nayo itakuwa safi."
54 [l]Haya ndiyo masharti kuhusu aina
yoyote ya ugonjwa wa ngozi wa kuambukiza,
mwasho wowote, 55 [m]upele ndani ya nguo au

[a]**14:31** Law 5:7; 15:15, 30
[b]**14:32** Law 13:2; 14:34; Mwa 12:5; 17:8; 48:4; Kut 6:4; Hes 13:2; 27:12; 32:22; Kum 3:27; 32:49; Isa 45:7; Amo 3:6
[c]**14:35** Za 91:10; Mit 3:33; Zek 5:4
[d]**14:36** Hes 19:18; Za 51:7; Isa 52:11; 1Tim 5:22; Ufu 18:4
[e]**14:37** Law 13:19; 14:38; 13:4-5
[f]**14:44** Law 13:51
[g]**14:46** Law 11:24; 17:15; 22:6; Hes 19:7-10; 1Kor 15:33
[h]**14:47** Law 11:25
[i]**14:48** Law 13:6; Kum 32:29; Ay 5:18; Hos 6:1; Mk 5:29; Lk 7:21
[j]**14:49** 1Fal 4:33
[k]**14:51** Za 51:7; 1Fal 4:33
[l]**14:54** Law 13:2
[m]**14:55** Law 13:47-52

ndani ya nyumba, [56] [a]kwa uvimbe, vipele au kipaku king'aacho, [57] kupambanua wakati kitu fulani ni safi au najisi.

Haya ndiyo masharti kuhusu magonjwa ya ngozi ya kuambukiza na upele.

### *Kutokwa Na Umajimaji Usababishao Unajisi*

15 BWANA akawaambia Mose na Aroni, [2] [b]"Semeni na Waisraeli mwaambie: 'Wakati mtu yeyote anapotokwa na usaha mwilini, usaha huo ni najisi. [3] Iwe unaendelea kutiririka kutoka mwilini mwake au umeziba, utamfanya kuwa najisi. Hivi ndivyo usaha wake utakavyomletea unajisi:

[4] " 'Kitanda chochote atakacholalia mtu mwenye kutokwa na usaha kitakuwa najisi, na chochote atakachokalia kitakuwa najisi. [5] [c]Yeyote atakayegusa kitanda chake ni lazima afue nguo zake na aoge kwa maji, naye atakuwa najisi mpaka jioni. [6] Yeyote atakayeketi juu ya kitu chochote alichokalia mwenye kutokwa na usaha, ni lazima afue nguo zake, na aoge kwa maji, naye atakuwa najisi mpaka jioni.

[7] [d]" 'Yeyote atakayemgusa mtu mwenye kutokwa na usaha, ni lazima afue nguo zake na aoge kwa maji, naye atakuwa najisi mpaka jioni.

[8] [e]" 'Ikiwa mtu mwenye kutokwa na usaha atamtemea mate mtu yeyote ambaye ni safi, mtu huyo ni lazima afue nguo zake na aoge kwa maji, naye atakuwa najisi mpaka jioni.

[9] " 'Kila tandiko ambalo mtu huyo atalikalia wakati wa kupanda mnyama litakuwa najisi, [10] [f]na yeyote atakayegusa kitu chochote alichokuwa amekalia atakuwa najisi mpaka jioni. Yeyote atakayeinua vitu hivyo ni lazima afue nguo zake na aoge kwa maji, naye atakuwa najisi mpaka jioni.

[11] " 'Yeyote atakayeguswa na mtu anayetokwa na usaha bila kunawa mikono yake kwa maji, ni lazima afue nguo zake na aoge kwa maji, naye atakuwa najisi mpaka jioni.

[12] [g]" 'Chungu cha udongo kitakachoguswa na mtu huyo ni lazima kivunjwe, na kifaa chochote cha mbao kitaoshwa kwa maji.

[13] [h]" 'Wakati mtu atakapotakasika kutoka usaha wake, anapaswa kuhesabu siku saba kwa utakaso wake. Ni lazima afue nguo zake na aoge kwa maji safi, naye atatakasika. [14] [i]Siku ya nane, atachukua hua wawili au makinda mawili ya njiwa, aje mbele za BWANA kwenye ingilio la Hema la Kukutania, na kumpa kuhani. [15] [j]Kuhani atavitoa dhabihu, mmoja kwa ajili ya sadaka ya dhambi na huyo mwingine kwa ajili ya sadaka ya kuteketezwa. Kwa njia hii atafanya upatanisho mbele za BWANA kwa ajili ya huyo mtu kwa sababu ya kutokwa usaha kwake.

[16] [k]" 'Wakati mtu akitokwa na shahawa, ni lazima aoge mwili mzima kwa maji, na atakuwa najisi mpaka jioni. [17] Vazi lolote ama ngozi yoyote yenye shahawa juu yake ni lazima ioshwe kwa maji, na itakuwa najisi mpaka jioni. [18] Ikiwa mtu atalala na mwanamke, na kukawa na kutoka kwa shahawa, ni lazima wote waoge kwa maji, nao watakuwa najisi mpaka jioni.

[19] [l]" 'Ikiwa mwanamke atatokwa na damu ya kawaida ya mwezi, atakuwa najisi kwa siku saba, na yeyote atakayemgusa atakuwa najisi mpaka jioni.

[20] " 'Chochote atakacholalia wakati wake wa hedhi kitakuwa najisi, na chochote atakachokikalia kitakuwa najisi. [21] Yeyote atakayegusa kitanda chake ni lazima afue nguo zake na aoge kwa maji, naye atakuwa najisi mpaka jioni. [22] [m]Yeyote atakayegusa chochote atakachokalia ni lazima afue nguo zake na aoge kwa maji, naye atakuwa najisi mpaka jioni. [23] Kiwe ni kitanda ama

---

[a]**14:56** Law 13:2; 14:57; 10:10; Kut 15:26; Kum 24:8; Za 78:5; 119:96; Mit 6:23
[b]**15:2** Law 22:4; Hes 5:2; 2Sam 3:29; Mt 9:20; Mk 5:25; Lk 8:43
[c]**15:5** Law 11:24-25; 14:8; 17:15; Ebr 9:10
[d]**15:7** Law 22:4-5
[e]**15:8** Hes 12:14; Ay 30:10; 2Kor 7:1
[f]**15:10** Hes 19:10
[g]**15:12** Law 6:28; 11:32
[h]**15:13** Law 8:33; 14:8; Hes 12:14; 19:11
[i]**15:14** Law 14:22; Hes 6:10-14
[j]**15:15** Law 5:7; 14:18-19, 31; Ebr 9:14; 10:1
[k]**15:16** Kum 23:10-11; Law 22:4; 15:18; 1Sam 21:4
[l]**15:19** Law 12:2; Eze 36:17
[m]**15:22** 2Kor 7:1; Eze 36:17

chochote alichokuwa amekikalia, ikiwa mtu
yeyote atakigusa, atakuwa najisi mpaka
jioni.
24 [a]" 'Ikiwa mwanaume atalala naye na
ile damu ya mwezi ikamgusa, atakuwa
najisi kwa siku saba; kitanda chochote
atakachokilalia huyo mwanaume kitakuwa
najisi.
25 [b]" 'Ikiwa mwanamke atatokwa na
damu kwa siku nyingi zaidi ya siku zake za
mwezi, au amekuwa na damu inayoendelea
zaidi ya kipindi chake, atakuwa najisi
kwa kipindi chote cha shida hiyo, kama
ilivyokuwa katika siku za hedhi yake.
26 Kitanda chochote atakachokilalia huyo
mwanamke wakati anaendelea kutokwa na
damu kitakuwa najisi, kama kilivyokuwa
kitanda chake wakati wa siku zake za hedhi,
na chochote atakachokalia kitakuwa najisi,
kama wakati wake wa hedhi. 27 Yeyote
agusaye vitu hivyo atakuwa najisi; ni lazima
afue nguo zake na kuoga kwa maji, naye
atakuwa najisi mpaka jioni.
28 " 'Wakati atakapotakasika kutoka hedhi
yake, ni lazima ahesabu siku saba, na baada
ya hapo atakuwa safi kwa kawaida ya
ibada. 29 [c]Siku ya nane ni lazima achukue
hua wawili au makinda mawili ya njiwa, na
kumletea kuhani kwenye mlango wa Hema
la Kukutania. 30 Kuhani atatoa dhabihu,
mmoja kwa ajili ya sadaka ya dhambi,
na huyo mwingine kwa ajili ya sadaka
ya kuteketezwa. Kwa njia hii, atafanya
upatanisho kwa ajili yake mbele za BWANA
kwa sababu ya unajisi wa kutokwa damu
kwake.
31 [d]" 'Ni lazima uwatenge Waisraeli
kutokana na vitu ambavyo vinawafanya
najisi, ili wasife katika unajisi wao kwa
kunajisi makao yangu,[e] ambayo yapo
katikati yao.' "
32 Haya ni masharti kwa ajili ya mtu
mwenye kutokwa na usaha, kwa ajili
ya yeyote atakayetokwa na shahawa,
33 kwa ajili ya mwanamke katika siku
zake za hedhi, kwa ajili ya mwanaume au
mwanamke atokwaye na usaha, na kwa
ajili ya mwanaume alalaye na mwanamke
ambaye ni najisi kwa kawaida ya ibada.

### *Siku Ya Upatanisho*

16 [f]BWANA akasema na Mose baada ya
kifo cha wale wana wawili wa Aroni
waliokufa walipokaribia mbele za BWANA.
2 BWANA akamwambia Mose: "Mwambie
ndugu yako Aroni asije wakati wowote
atakavyo yeye ndani ya Patakatifu pa
Patakatifu, nyuma ya pazia pale mbele
ya kiti cha rehema kile kilichoko juu ya
Sanduku la Agano, la sivyo atakufa, kwa
sababu huwa ninatokea ndani ya wingu juu
ya kile kiti cha rehema.
3 [g]"Hivi ndivyo Aroni atakavyoingia
katika mahali patakatifu: atachukua fahali
mchanga kwa ajili ya sadaka ya dhambi,
na kondoo dume kwa ajili ya sadaka ya
kuteketezwa. 4 [h]Atavaa koti takatifu la
kitani, pamoja na nguo za ndani za kitani;
atafunga mshipi wa kitani kiunoni, na
kuvaa kilemba cha kitani. Haya ni mavazi
matakatifu, kwa hiyo ni lazima aoge kwa
maji kabla ya kuyavaa mavazi hayo.
5 [i]Atachukua mbuzi dume wawili kutoka
kwa jumuiya ya Israeli kwa ajili ya sadaka
ya dhambi, na kondoo dume kwa ajili ya
sadaka ya kuteketezwa.
6 [j]"Aroni atamtoa huyo fahali kwa ajili ya
sadaka yake ya dhambi ili afanye upatanisho
kwa ajili yake mwenyewe na nyumba yake.
7 Kisha atawachukua wale mbuzi dume
wawili na kuwaleta mbele za BWANA
kwenye ingilio la Hema la Kukutania.

---

[a]**15:24** Law 12:2; 18:19; 20:18; Eze 18:6
[b]**15:25** Mt 9:20; Lk 8:43; Mk 5:25
[c]**15:29** Law 14:22; 15:30; 5:10; 14:20, 31; 18:19; 2Sam 11:4; Mk 5:25; Lk 8:43
[d]**15:31** Law 20:3; Hes 5:3; 19:13, 20; 2Sam 15:25; 2Fal 21:7; Za 33:14; 74:7; 76:2; Eze 5:11; 23:38
[e]31 Yaani *maskani ya Mungu.*
[f]**16:1** Law 10:1; 16:2; Kut 26:33-34; 25:22; 30:10; 40:34; Ebr 9:7, 25; 10:19; 6:19; 2Sam 22:10
[g]**16:3** Law 4:1-12; Ebr 9:24-25
[h]**16:4** Kut 28:29, 42; 29:4, 29-30; Law 21:10; Hes 20:26-28; Ebr 10:22; Eze 9:2; 44:17-18
[i]**16:5** Law 4:3, 13-21; 2Nya 29:23; Za 50:9; Ezr 6:17; Eze 45:22
[j]**16:6** Law 9:7; Ebr 7:27; 9:7-12

8 [a]Aroni atapiga kura kwa ajili ya hao mbuzi
wawili, mmoja kwa ajili ya Bwana na
mwingine kwa ajili ya kubebeshwa dhambi.[b]
9 Aroni atamleta yule mbuzi ambaye kura
ya Bwana imemwangukia na kumtoa
dhabihu kwa ajili ya sadaka ya dhambi.
10 [c]Lakini mbuzi aliyechaguliwa kwa kura
kuwa wa kubebeshwa dhambi atatolewa
akiwa hai mbele za Bwana, atumike kwa
kufanya upatanisho kwa kumwacha aende
jangwani akiwa amebebeshwa dhambi.

11 [d]"Aroni atamleta yule fahali kwa ajili
ya sadaka ya dhambi yake mwenyewe,
ili kufanya upatanisho kwa ajili yake
na nyumba yake, naye atamchinja huyo
fahali kwa ajili ya sadaka ya dhambi
yake mwenyewe. 12 [e]Atachukua chetezo
kilichojaa makaa yanayowaka kutoka
madhabahuni mbele za Bwana, na konzi
mbili za uvumba laini uliosagwa vizuri
wenye harufu, na kuvipeleka nyuma ya
pazia. 13 [f]Ataweka uvumba juu ya moto
mbele za Bwana, na moshi wa uvumba
utafunika kile kiti cha rehema kilicho juu ya
Ushuhuda, ili asife. 14 [g]Atachukua sehemu
ya damu ya fahali, na kwa kidole chake
atanyunyiza sehemu ya mbele ya kiti cha
rehema; kisha atanyunyiza sehemu ya hiyo
damu kwa kidole chake mara saba mbele
ya kiti cha rehema.

15 [h]"Kisha atamchinja mbuzi wa sadaka
ya dhambi kwa ajili ya watu, na kuichukua
damu yake nyuma ya pazia, na aifanyie
kama alivyofanya kwa damu ya fahali:
Atanyunyiza juu ya kiti cha rehema na mbele
yake. 16 [i]Kwa njia hii atafanya upatanisho
kwa ajili ya Patakatifu pa Patakatifu kwa
sababu ya unajisi na uasi wa Waisraeli, kwa
dhambi zao zozote. Atafanya hivyo kwa
ajili ya Hema la Kukutania, ambalo liko
miongoni mwao katikati ya unajisi wao.
17 Mtu yeyote haruhusiwi kuwa ndani ya
Hema la Kukutania, kuanzia wakati Aroni
anapoingia kufanya upatanisho katika
Patakatifu pa Patakatifu, hadi atakapotoka
nje, baada ya kujifanyia upatanisho yeye
mwenyewe na nyumba yake, pamoja na
jumuiya yote ya Israeli.

18 [j]"Kisha atatoka aje kwenye madhabahu
yaliyo mbele za Bwana na kufanya
upatanisho kwa ajili yake. Atachukua
sehemu ya damu ya fahali na sehemu ya
damu ya mbuzi, na kuiweka kwenye pembe
za madhabahu. 19 [k]Atanyunyiza baadhi ya
hiyo damu juu ya madhabahu kwa kidole
chake mara saba, ili kuitakasa na kuiweka
wakfu kutokana na unajisi wa Waisraeli.

20 "Aroni atakapokuwa amemaliza
kufanya upatanisho kwa ajili ya Patakatifu
pa Patakatifu, Hema la Kukutania na
madhabahu, atamleta mbele yule mbuzi
aliye hai. 21 [l]Aroni ataweka mikono yake
miwili juu ya kichwa cha mbuzi aliye
hai na kuungama juu yake uovu wote
na uasi wa Waisraeli, yaani dhambi zao
zote, ili kuziweka juu ya kichwa cha huyo
mbuzi. Atamwachia huyo mbuzi akimbilie
jangwani kwa uangalizi wa mtu aliyepewa
wajibu huo. 22 [m]Yule mbuzi atachukua
juu yake dhambi zao zote mpaka mahali
pasipo na watu; naye yule mtu atamwachia
akimbilie jangwani.

23 [n]"Kisha Aroni ataenda ndani ya Hema
la Kukutania na kuvua yale mavazi ya
kitani aliyoyavaa kabla ya kuingia katika
Patakatifu pa Patakatifu, naye atayaacha
pale. 24 [o]Ataoga kwa maji katika mahali
patakatifu na kuvaa mavazi yake ya

[a]**16:8** Hes 26:55-56; 33:54; 34:13; Yos 14:2; 18:6; Amu 20:9; Neh 10:34; Es 3:7; 9:24; Za 22:18; Mit 16:33
[b]8 Yaani *Azazeli*, maana yake *mbuzi wa ondoleo la dhambi*; pia ms. 10, 26.
[c]**16:10** Isa 53:4-10; Rum 3:25; 1Yn 2:2
[d]**16:11** Ebr 9:7
[e]**16:12** Law 10:1; Ufu 8:5; Kut 25:6; 30:34-38
[f]**16:13** Kut 25:17; 28:43; Law 22:9; Kut 31:7-8; Hes 16:7, 18; Ufu 8:3-4
[g]**16:14** Law 4:5-6; Ebr 9:7-13, 25
[h]**16:15** Law 4:7, 13-21; Ebr 9:3, 7-12; 13:11; 7:27; Hes 19:19; Isa 52:15; Eze 36:25
[i]**16:16** Kut 26:33; 29:4, 36; 40:2; Rum 3:25; Ebr 9:25
[j]**16:18** Law 4:7, 24-25
[k]**16:19** Eze 43:20; Ebr 9:12
[l]**16:21** Kut 29:10; Law 5:5
[m]**16:22** Kut 28:38; Isa 53:12; Za 103:1-13; Mt 8:17; Yn 1:29; 1Pet 2:24
[n]**16:23** Kut 28:42; Eze 42:14; Flp 2:6-11
[o]**16:24** Law 6:16; 1:3; 16:25; Kut 29:13; Law 4:10

kawaida. Kisha atatoka na kutoa dhabihu
ya sadaka ya kuteketezwa kwa ajili yake
na sadaka ya kuteketezwa kwa ajili ya
watu, ili kufanya upatanisho kwa ajili yake
mwenyewe, na kwa ajili ya watu. 25 Pia
atachoma mafuta ya mnyama wa sadaka
ya dhambi juu ya madhabahu.
26 [a]“Yule mtu anayemwachia yule mbuzi
wa kubebeshwa dhambi ni lazima afue
nguo zake na kuoga kwa maji; baadaye
anaweza kuingia kambini. 27 [b]Yule fahali na
mbuzi waliotolewa kwa ajili ya sadaka za
dhambi, ambao damu yao ilikuwa imeletwa
Patakatifu pa Patakatifu kwa ajili ya
kufanya upatanisho, ni lazima watolewe nje
ya kambi. Ngozi zao, nyama, na matumbo
pamoja na mavi vitateketezwa kwa moto.
28 [c]Mtu atakayevichoma ni lazima afue
nguo zake na aoge kwa maji; baadaye
ataweza kuingia kambini.
29 [d]“Hili litakuwa agizo la kudumu kwa
ajili yenu: Katika siku ya kumi ya mwezi
wa saba ni lazima mfunge, wala msifanye
kazi yoyote, iwe mzawa au mgeni anayeishi
miongoni mwenu, 30 [e]kwa sababu siku hii
upatanisho utafanyika kwa ajili yenu ili
kuwatakasa. Kisha mtakuwa safi mbele za
BWANA kutokana na dhambi zenu zote.
31 [f]Ni Sabato ya mapumziko, na lazima
mfunge; ni agizo la kudumu. 32 [g]Kuhani
ambaye ametiwa mafuta na kuwekwa
wakfu ili kuingia mahali pa baba yake
kama kuhani mkuu atafanya upatanisho.
Atavaa mavazi matakatifu ya kitani, 33 [h]na
kufanya upatanisho kwa ajili ya Patakatifu
pa Patakatifu, Hema la Kukutania na
madhabahu, na pia kwa ajili ya makuhani,
pamoja na jumuiya yote ya watu.
34 [i]“Hili litakuwa agizo la kudumu kwa
ajili yenu: Upatanisho utafanywa mara
moja tu kwa mwaka kwa ajili ya dhambi
zote za Waisraeli.”

Ndivyo ilivyofanyika, kama vile BWANA
alivyomwamuru Mose.

*Kunywa Damu Kumekatazwa*

17 BWANA akamwambia Mose, 2 [j]“Sema
na Aroni na wanawe, pamoja na
Waisraeli wote, uwaambie: ‘Hili ndilo
BWANA aliloagiza: 3 [k]Mwisraeli yeyote
atakayetoa dhabihu ya maksai, mwana-
kondoo au mbuzi ndani ya kambi au nje
yake, 4 [l]badala ya kuileta kwenye ingilio la
Hema la Kukutania ili kuileta kama sadaka
kwa BWANA mbele ya Maskani ya BWANA,
mtu huyo atahesabiwa kuwa na hatia
ya kumwaga damu; ni lazima akatiliwe
mbali na watu wake. 5 [m]Hii ni ili Waisraeli
wamletee BWANA dhabihu wanazozifanya
sasa mahali pa wazi mashambani. Ni lazima
wazilete kwa makuhani, yaani kwa BWANA,
katika ingilio la Hema la Kukutania, na
kutoa dhabihu kama sadaka za amani.
6 Kuhani atanyunyiza damu kwenye
madhabahu ya BWANA katika ingilio la
Hema la Kukutania, na kuyateketeza mafuta
ya hiyo dhabihu kuwa harufu nzuri ya
kumpendeza BWANA. 7 [n]Hawatatoa kamwe
dhabihu zao kwa sanamu za mbuzi ambazo
wamekuwa wakijifanyia nazo ukahaba. Hili
litakuwa agizo la kudumu kwao na kwa ajili
ya vizazi vijavyo.’
8 “Waambie: ‘Mwisraeli yeyote au
mgeni yeyote anayeishi miongoni mwao
atakayetoa sadaka ya kuteketezwa au
dhabihu 9 [o]bila kuileta kwenye ingilio la

---

[a]**16:26** Law 11:25; 14:8; Ebr 9:10
[b]**16:27** Kut 29:14; Ebr 13:11; Law 8:17; 4:12
[c]**16:28** Hes 19:8-10
[d]**16:29** Kut 12:14, 19; 31:15; Law 25:9; 23:27, 28, 32; Hes 29:7; Isa 58:3
[e]**16:30** Kut 30:10; Za 51:2; Yer 33:8; Eze 36:33; Zek 13:1; Efe 5:26
[f]**16:31** Ezr 8:21; Isa 58:3-5; Dan 10:12; Mdo 27:9
[g]**16:32** Kut 30:30; 28:2; Hes 20:26
[h]**16:33** Eze 45:18
[i]**16:34** Kut 27:21; Ebr 9:7, 25; Law 23:31; Hes 29:7
[j]**17:2** Law 10:6, 12
[k]**17:3** Law 3:7; 7:23
[l]**17:4** 1Fal 8:4; 2Nya 1:3; Kum 12:5-21; Mwa 17:14
[m]**17:5** Law 3:1; Eze 43:27; Mwa 21:33; 22:2; 1Fal 14:22-23
[n]**17:7** Kut 12:14; 22:20; 34:15; 34:15; Yer 3:6-9; Eze 23:3; 1Kor 10:20; Mwa 9:12; Kum 32:17; 2Nya 11:15; Za 106:37
[o]**17:9** Law 1:3; 3:7

Hema la Kukutania ili kutoa dhabihu kwa
BWANA, mtu huyo ni lazima akatiliwe
mbali na watu wake.
10 [a]“ ‘Mwisraeli yeyote au mgeni anayeishi
miongoni mwao ambaye atakunywa damu
yoyote, nitakuwa kinyume cha mtu huyo
atakayekunywa damu na kumkatilia mbali
na watu wake. 11 [b]Kwa kuwa uhai wa
kiumbe uko ndani ya damu, nami nimewapa
hiyo damu ili mfanyie upatanisho kwa ajili
yenu wenyewe juu ya madhabahu; damu
ndiyo ifanyayo upatanisho kwa ajili ya
maisha ya mtu. 12 Kwa hiyo, ninawaambia
Waisraeli, “Hakuna hata mmoja wenu
anayeruhusiwa kunywa damu, wala mgeni
anayeishi miongoni mwenu haruhusiwi
kunywa damu.”
13 [c]“ ‘Mwisraeli yeyote au mgeni anayeishi
miongoni mwenu ambaye atamwinda
mnyama au ndege anayeruhusiwa kuliwa
ni lazima aimwage damu na kuifunika
kwa udongo, 14 [d]kwa sababu uhai wa kila
kiumbe ni katika damu yake. Ndiyo sababu
nimewaambia Waisraeli, “Kamwe msinywe
damu ya kiumbe chochote, kwa sababu
uhai wa kila kiumbe ni katika damu yake;
yeyote atakayekunywa damu ni lazima
akatiliwe mbali.”
15 [e]“ ‘Mtu yeyote, awe mzawa au mgeni,
ambaye atakula mzoga wa kitu chochote
ama kilichouawa na wanyama mwitu ni
lazima afue nguo zake na aoge kwa maji,
naye atakuwa najisi kwa kawaida ya ibada
mpaka jioni, kisha atakuwa safi. 16 [f]Lakini
kama hakufua nguo zake na kuoga, atakuwa
na hatia kwa kosa hilo.’ ”

[a]**17:10** Mwa 9:4; Kum 12:16, 23; 1Sam 14:33; Law 26:17; Yer 44:11; Eze 15:7
[b]**17:11** Mwa 9:4; Ebr 9:22
[c]**17:13** Law 7:26; Eze 24:7; 33:25; Mdo 15:20; Kum 12:16
[d]**17:14** Mwa 9:4; Law 7:24; 14:8; 11:40; Kol 1:14; Kum 14:21; Kut 22:31; Mk 14:24; Rum 5:9
[e]**17:15** Kut 22:31; Kum 14:2; Eze 4:14
[f]**17:16** Law 5:1; Hes 19:20; Ebr 9:28

### *Uhusiano Wa Kukutana Kimwili Kinyume Cha Sheria*

18 BWANA akamwambia Mose, 2 [g]“Sema
na Waisraeli uwaambie: ‘Mimi
ndimi BWANA Mungu wenu. 3 [h]Msifanye
kama wafanyavyo huko Misri, mahali
mlipokuwa mnaishi, wala msifanye kama
wanavyofanya katika nchi ya Kanaani,
mahali ninapowapeleka. Msifuate matendo
yao. 4 [i]Ni lazima mzitii sheria zangu, na mwe
waangalifu kuzifuata amri zangu. Mimi
ndimi BWANA Mungu wenu. 5 [j]Zishikeni
amri zangu na sheria zangu, kwa maana
mtu anayezitii ataishi kwa hizo. Mimi ndimi
BWANA.
6 “ ‘Hakuna mtu awaye yote
atakayemsogelea ndugu wa karibu ili
kukutana naye kimwili. Mimi ndimi
BWANA.
7 [k]“ ‘Usimvunjie heshima baba yako kwa
kukutana kimwili na mama yako. Yeye ni
mama yako; usiwe na mahusiano kama
hayo naye.
8 [l]“ ‘Usikutane kimwili na mke wa baba
yako; hiyo itamvunjia heshima baba yako.
9 [m]“ ‘Usikutane kimwili na dada yako,
wala binti wa baba yako, au binti wa mama
yako, awe amezaliwa katika nyumba hiyo
au mahali pengine.
10 “ ‘Usikutane kimwili na binti wa
mwanao ama binti wa binti yako; utajivunjia
heshima.
11 “ ‘Usikutane kimwili na binti wa mke
wa baba yako, aliyezaliwa na baba yako;
huyo ni dada yako.
12 [n]“ ‘Usikutane kimwili na dada wa baba
yako; ni ndugu wa karibu wa baba yako.

[g]**18:2** Mwa 17:7; Eze 20:5; Kut 6:7
[h]**18:3** Kut 23:24; Kum 18:9; 2Fal 16:3; 17:8; 1Nya 5:25; Eze 23:8
[i]**18:4** Mwa 26:5; Kum 4:1; 1Fal 11:11; Yer 44:10, 23; Eze 11:12
[j]**18:5** Mwa 26:5; Neh 9:20; Isa 55:2; Eze 18:9; 20:11; Amo 5:4-6; Mt 19:17; Rum 10:5; Gal 3:12
[k]**18:7** Law 20:11; Kum 27:20; Eze 22:10-11
[l]**18:8** 1Kor 5:11; Mwa 35:22; Law 20:11; Kum 22:30; 27:20
[m]**18:9** Law 20:17; Kum 27:22; 2Sam 13:13; Eze 22:11
[n]**18:12** Law 20:19

13 [a]“ ‘Usikutane kimwili na dada wa mama
yako, kwa sababu ni ndugu wa mama yako
wa karibu.
14 “ ‘Usimvunjie heshima ndugu wa baba
yako, kwa kukutana kimwili na mke wake;
yeye ni shangazi yako.
15 [b]“ ‘Usikutane kimwili na mkwe wako,
yeye ni mke wa mwanao; usiwe na
mahusiano kama hayo naye.
16 [c]“ ‘Usikutane kimwili na mke wa kaka
yako; utamvunjia heshima kaka yako.
17 [d]“ ‘Usikutane kimwili na mwanamke
kisha na binti yake. Usikutane kimwili na
binti wa mwanawe au binti wa binti yake;
hao ni ndugu zake wa karibu. Huo ni uovu.
18 [e]“ ‘Usimchukue dada wa mke wako
kuwa mke mwenza, na kukutana naye
kimwili wakati bado mke wako anaishi.
19 [f]“ ‘Usimsogelee mwanamke ili kukutana
naye kimwili wakati wa unajisi wa siku
zake za mwezi.
20 [g]“ ‘Usikutane kimwili na mke wa jirani
yako na kujitia naye unajisi.
21 [h]“ ‘Usimtoe mtoto wako yeyote
awe kafara kwa mungu Moleki, kwani
hutalinajisi kamwe jina la Mungu wako.
Mimi ndimi BWANA.
22 [i]“ ‘Usikutane kimwili na mwanaume
kama mtu akutanaye na mwanamke; hilo
ni chukizo.
23 [j]“ ‘Usikutane kimwili na mnyama
na kujitia unajisi kwake. Mwanamke
asijipeleke kwa mnyama ili kukutana naye
kimwili; huo ni upotovu.
24 [k]“ ‘Msijitie unajisi kwa njia yoyote
katika hizi, kwa sababu hivi ndivyo mataifa
nitakayoyafukuza mbele yenu yalivyojitia
unajisi. 25 [l]Hata nchi ilitiwa unajisi, hivyo
nikaiadhibu kwa dhambi zake, nayo nchi
ikawatapika wakazi wake. 26 [m]Lakini ni
lazima uzitunze amri zangu na sheria
zangu. Mzawa na wageni waishio miongoni
mwenu kamwe wasifanye mambo yoyote ya
machukizo haya, 27 kwa kuwa mambo haya
yote yalifanywa na watu walioishi katika
nchi hii kabla yenu, na nchi ikawa najisi.
28 Kama mkiinajisi nchi, itawatapika kama
ilivyowatapika mataifa yaliyowatangulia.
29 “ ‘Kila mtu atakayefanya mojawapo
ya machukizo haya, watu hao ni lazima
wakatiliwe mbali na watu wao. 30 [n]Shikeni
maagizo yangu, wala msifuate desturi za
machukizo yoyote yaliyofanywa kabla
hamjafika katika nchi hii, na kujitia unajisi
kwa hayo. Mimi ndimi BWANA Mungu
wako.’ ”

*Sheria Mbalimbali*

19 BWANA akamwambia Mose, 2 “Sema na
kusanyiko lote la Israeli na uwaambie:
‘Kuweni watakatifu, kwa kuwa mimi,
BWANA Mungu wenu, ni mtakatifu.
3 [o]“ ‘Kila mmoja wenu ni lazima
amheshimu mama yake na baba yake, na
pia ni lazima kuzishika Sabato zangu. Mimi
ndimi BWANA Mungu wenu.
4 [p]“ ‘Msiabudu sanamu, wala
msijitengenezee miungu ya shaba. Mimi
ndimi BWANA Mungu wenu.
5 “ ‘Mnapotoa dhabihu ya sadaka ya amani

[a]**18:13** Law 20:20
[b]**18:15** Mwa 11:31; 38:16; Eze 22:11; Law 20:12
[c]**18:16** Law 20:21; Mt 14:4; Mk 6:18
[d]**18:17** Law 20:14; Kum 27:23
[e]**18:18** Mwa 30:1; Mal 2:15
[f]**18:19** Law 15:24-30; 20:18; Eze 18:6
[g]**18:20** Kut 20:14; Mt 5:27-28; 1Kor 6:9; Ebr 13:4; Mit 6:29
[h]**18:21** Kum 9:4; 12:31; 18:10; 2Fal 16:3; 17:17; 21:6; 23:10; 2Nya 28:1-4; 33:6; Za 106:37-38; Isa 48:11; 57:5; Yer 7:30-31; 19:5; 32:35; Eze 16:20; 22:26; 36:20; Mik 6:7; Law 19:12; 20:2-5; 21:6; Amo 2:7; 1Fal 11:5, 7, 33; Sef 1:5; Mal 1:12; Kut 6:2
[i]**18:22** Law 20:13; Kum 23:18; Rum 1:27; 1Kor 6:9; Mwa 19:5
[j]**18:23** Kut 22:19; Law 20:15; Kum 27:21
[k]**18:24** Law 20:23; Kum 9:4; 18:12; Mt 15:18; 1Kor 3:17
[l]**18:25** Hes 35:34; Kum 9:5; 12:31; 18:12; 21:23; Law 20:23; Ay 20:15; Yer 51:34
[m]**18:26** Mwa 26:5; 18:28; Law 20:22; Ezr 9:11; Mao 1:17
[n]**18:30** Law 8:35; Kum 11:1; 19:2; Hes 14:5; Za 68:26; Kut 20:2; 15:11; 1Pet 1:16; Law 11:44; 20:26
[o]**19:3** Kut 20:8, 12; Law 11:44; Neh 9:14; 13:15-21; Isa 58:13; Mk 2:27
[p]**19:4** Kut 20:4; Amu 17:3; Za 96:5; 115:4-7; 135:15; 1Kor 10:14

kwa Bwana, toeni kwa namna ambayo
itakubaliwa kwa niaba yenu. 6 [a]Sadaka hiyo
italiwa siku iyo hiyo mnayoitoa, au kesho
yake; chochote kitakachobaki hadi siku ya
tatu lazima kiteketezwe kwa moto. 7 Kama
sehemu yoyote ya sadaka hiyo italiwa siku
ya tatu, itakuwa si safi, nayo haitakubaliwa.
8 [b]Yeyote atakayekula atawajibishwa, kwa
sababu amenajisi kitu kilicho kitakatifu kwa
Bwana; mtu huyo lazima akatiliwe mbali
na watu wake.

9 [c]“ ‘Wakati uvunapo mavuno ya nchi
yako, usivune hadi kwenye mipaka ya
shamba lako, wala usikusanye mabaki
ya mavuno yako. 10 [d]Usirudi mara ya pili
katika shamba lako la mizabibu, wala
usiokote zabibu zilizoanguka chini. Ziache
kwa ajili ya maskini na mgeni. Mimi ndimi
Bwana Mungu wako.

11 [e]“ ‘Usiibe.

“ ‘Usiseme uongo.

“ ‘Msidanganyane.

12 [f]“ ‘Usiape kwa uongo kwa Jina langu,
na hivyo kulinajisi jina la Mungu wako.
Mimi ndimi Bwana.

13 [g]“ ‘Usimdhulumu wala kumwibia jirani
yako.

“ ‘Usishikilie mshahara wa kibarua usiku
kucha hadi asubuhi.

14 [h]“ ‘Usimlaani kiziwi, wala usiweke
kikwazo mbele ya kipofu, lakini umche
Mungu wako. Mimi ndimi Bwana.

15 [i]“ ‘Usipotoshe haki; usionyeshe
kumpendelea maskini, wala upendeleo
kwa mwenye cheo, bali mwamulie jirani
yako kwa haki.

16 [j]“ ‘Usieneze uchochezi miongoni mwa
watu wako.

“ ‘Usifanye kitu chochote kile
kinachohatarisha maisha ya jirani yako.
Mimi ndimi Bwana.

17 [k]“ ‘Usimchukie ndugu yako moyoni
mwako. Karipia jirani yako kwa uwazi ili
usishiriki hatia yake.

18 [l]“ ‘Usijilipizie kisasi wala kuwa na
kinyongo dhidi ya mmoja wa jamaa
yako, lakini mpende jirani yako kama
unavyojipenda wewe mwenyewe. Mimi
ndimi Bwana.

19 [m]“ ‘Mtazishika amri zangu.

“ ‘Usiwaache wanyama wako wa kufugwa
wakazaana na wengine wa aina tofauti.

“ ‘Usipande mbegu za aina mbili katika
shamba lako.

“ ‘Usivae nguo iliyofumwa kwa nyuzi za
aina mbili tofauti.

20 [n]“ ‘Kama mwanaume anakutana
kimwili na mwanamke ambaye ni msichana
mtumwa aliyeposwa na mwanaume
mwingine, lakini ambaye hajakombolewa
wala hajapewa uhuru, lazima iwepo adhabu
inayofaa. Hata hivyo hawatauawa, kwa
sababu msichana alikuwa bado hajaachwa
huru. 21 [o]Lakini huyo mtu lazima alete
kondoo dume kwenye ingilio la Hema la
Kukutania kwa ajili ya sadaka ya hatia
kwa Bwana. 22 Kupitia kwa huyo kondoo
dume wa sadaka ya hatia, kuhani atafanya

[a]**19:6** Law 7:16-18
[b]**19:8** Law 22:2, 15-16; Hes 18:32; Mwa 17:14
[c]**19:9** Rut 2:2-7; Law 23:10, 22; Kum 24:19-22; Ay 24:10; Kut 23:11; Kum 15:1-18
[d]**19:10** Kum 24:19-22; Za 140:12; Mit 14:31; Isa 3:12-15; Mhu 5:8
[e]**19:11** Kut 20:15-16; 23:4; Lk 3:14; Efe 4:25; Law 6:2; 1Fal 13:18; Yer 9:3-5; Mdo 5:3-4
[f]**19:12** Yer 5:2; 7:9; 34:16; 44:16, 26; Mal 3:5; Kut 3:13; 20:7; Kum 18:19; Mit 18:10; Isa 42:8; Mt 5:33
[g]**19:13** Law 25:14, 17; Kut 20:15; 22:15, 25-27; Ay 7:2; 24:12; 31:39; Isa 16:14; Mal 3:5; Kum 24:15; Yer 22:13; Mt 20:8; 1Tim 5:18; Yak 5:4
[h]**19:14** Kut 4:11; Law 21:18; 25:17, 36; Kum 27:18; Rum 14:13; 1Pet 2:17
[i]**19:15** Kut 13:2; 23:8; Kum 24:17; Ay 13:8, 10; 32:21; 34:19; Mit 24:23; 28:21; Mal 2:9; Yak 2:1-4
[j]**19:16** Za 15:3, 5; 31:13; 41:6; 101:5; Yer 6:28; 9:4; Eze 22:9, 12; Kut 23:7; Kum 10:17; 27:25
[k]**19:17** 1Yn 2:9; Mt 18:15; Lk 17:3; Mwa 27:41
[l]**19:18** Mwa 4:23; Rum 12:19; 13:9; Ebr 10:30; Za 103:9; Kut 20:16; Mt 5:43; 19:16; 22:39; Mk 12:31; Lk 10:27; Yn 13:34; Gal 5:14; Yak 2:8
[m]**19:19** Mwa 26:5; Kum 22:9, 11
[n]**19:20** Kum 22:23-27
[o]**19:21** Law 5:15

upatanisho kwa ajili yake mbele za Bwana kwa ajili ya dhambi aliyotenda, naye atasamehewa dhambi yake.

23 “ ‘Mtakapoingia katika hiyo nchi na kupanda aina yoyote ya mti wa matunda, hesabuni matunda yake kama yaliyokatazwa. Kwa miaka mitatu mtayahesabu kwamba yamekatazwa; hayaruhusiwi kuliwa. 24 [a]Katika mwaka wa nne matunda yote ya mti huo yatakuwa matakatifu, sadaka ya sifa kwa Bwana. 25 Bali katika mwaka wa tano mnaweza kula matunda ya mti huo. Kwa njia hii mavuno yenu yataongezewa. Mimi ndimi Bwana Mungu wako.

26 [b]“ ‘Msile nyama yoyote yenye damu ndani yake.

“ ‘Msifanye uaguzi wala uchawi.

27 [c]“ ‘Msikate nywele za kichwa denge, wala kunyoa pembe za ndevu zenu.

28 [d]“ ‘Msichanje chale miili yenu kwa ajili ya mfu, wala msijichore alama juu ya miili yenu. Mimi ndimi Bwana.

29 [e]“ ‘Usimdhalilishe binti yako kwa kumfanya kahaba, la sivyo nchi itageukia ukahaba na kujaa uovu.

30 [f]“ ‘Shika Sabato zangu na kuheshimu mahali pangu patakatifu. Mimi ndimi Bwana.

31 [g]“ ‘Msiende kwa waaguzi, wala msitafute wapunga pepo, kwa maana watawanajisi. Mimi ndimi Bwana Mungu wako.

32 [h]“ ‘Uwapo mbele ya mzee, simama ili kuonyesha heshima kwa wazee, nawe umche Mungu wako. Mimi ndimi Bwana.

33 “ ‘Wakati mgeni anaishi pamoja nawe katika nchi yako, usimnyanyase. 34 [i]Mgeni anayeishi pamoja nawe ni lazima umtendee kama mmoja wa wazawa wa nchi yako. Mpende kama unavyojipenda mwenyewe, kwa maana ulikuwa mgeni katika nchi ya Misri. Mimi ndimi Bwana Mungu wako.

35 [j]“ ‘Usitumie vipimo vya udanganyifu unapopima urefu, kupima uzito, wala kupima wingi. 36 [k]Tumia mizani halali, mawe ya kupimia uzito halali, efa[l] halali, na hini[m] halali. Mimi ndimi Bwana Mungu wako, ambaye alikutoa katika nchi ya Misri.

37 [n]“ ‘Shika amri zangu zote na sheria zangu zote, nawe uzifuate. Mimi ndimi Bwana.’ ”

### *Adhabu Kwa Ajili Ya Dhambi*

20 Bwana akamwambia Mose, 2 [o]“Sema na wana wa Israeli: ‘Mwisraeli yeyote au mgeni anayeishi katika Israeli ambaye atamtoa yeyote miongoni mwa watoto wake kuwa sadaka kwa mungu Moleki, mtu huyo lazima auawe. Watu wa jumuiya hiyo watampiga kwa mawe. 3 [p]Mimi nitauelekeza uso wangu dhidi ya mtu huyo, nami nitamkatilia mbali na watu wake. Kwa maana kwa kumtoa mmoja wa watoto wake kwa mungu Moleki, amenajisi madhabahu yangu na kulinajisi Jina langu takatifu. 4 [q]Ikiwa watu wa jumuiya watafumba macho wakati mtu huyo anapomtoa mmoja wa watoto wake kwa mungu Moleki, nao

---

[a] **19:24** Kut 22:29; Mit 3:9; Kum 12:17-18
[b] **19:26** Mwa 9:4; 30:27; Isa 44:25; Eze 22:18; 2Fal 17:17
[c] **19:27** Law 21:5; 2Sam 10:4-5; Yer 41:5; 48:37; Eze 5:1-5; Yer 9:26
[d] **19:28** Law 21:5; 1Fal 18:28; Yer 16:6; 41:5; 47:5
[e] **19:29** Law 21:9; Kum 23:18; Mwa 34:7
[f] **19:30** Kut 20:8; Law 26:2
[g] **19:31** Kut 22:18; 1Sam 28:7-20; 1Nya 10:13; Law 20:6; 2Fal 21:6; 23:24; Isa 8:19; 19:3; 29:4; 47:12; 65:4
[h] **19:32** 1Fal 12:8; Ay 29:8; 32:4; Mit 23:22; Mao 5:12; 1Tim 5:1; Law 11:44
[i] **19:34** Kut 12:48; 22:21; 23:9; Kum 10:19; 23:7; Za 146:9
[j] **19:35** Kum 25:13-16
[k] **19:36** Ay 31:6; Mit 11:1; 20:10; Hes 12:7; Mik 6:11; Amu 6:19; Rut 2:17; 1Sam 1:24; 17:17; Eze 45:10-11; Kum 25:13-15; Kut 12:17
[l] 36 Efa kilikuwa kipimo cha vitu vikavu.
[m] 36 Hini kilikuwa kipimo cha vitu vimiminika.
[n] **19:37** 2Fal 17:37; 2Nya 7:17; Za 119:5; Eze 18:9; Mwa 26:5; Kum 6:25; Law 18:4-5
[o] **20:2** Mwa 26:11; Kut 19:21; Law 24:14; Hes 15:35-36; Kum 21:21; Yos 7:25; 2Fal 17:17; 23:10; 2Nya 33:6
[p] **20:3** Law 23:30; 15:31; 18:21; Za 74:7; 79:1; Yer 7:30; Eze 5:11; Hes 19:20
[q] **20:4** Kum 17:2-5

wakaacha kumuua, 5 [a]mimi nitauelekeza
uso wangu dhidi ya mtu huyo pamoja
na jamaa yake, nami nitawakatilia mbali
yeye na watu wote waliofanya ukahaba na
Moleki.
6 [b]“ ‘Mimi nitauelekeza uso wangu dhidi
ya mtu anayeenda kwa waaguzi na wenye
pepo, na hivyo kujifanyia ukahaba kwa
kuwafuata, nami nitamkatilia mbali na
watu wake.
7 [c]“ ‘Jitakaseni basi, nanyi kuweni
watakatifu, kwa sababu mimi ndimi
BWANA Mungu wenu. 8 [d]Shikeni amri
zangu na kuzifuata. Mimi ndimi BWANA,
niwafanyaye ninyi watakatifu.
9 [e]“ ‘Ikiwa mtu yeyote atamlaani baba
yake au mama yake, lazima auawe.
Amemlaani baba yake au mama yake, nayo
damu yake itakuwa juu ya kichwa chake
mwenyewe.
10 [f]“ ‘Ikiwa mtu atazini na mke wa mtu
mwingine, yaani mke wa jirani yake,
wazinzi hao wawili lazima wauawe.
11 [g]“ ‘Kama mtu atakutana kimwili na mke
wa baba yake, hakumheshimu baba yake.
Mwanaume huyo na mwanamke huyo wote
wauawe; damu yao itakuwa juu ya vichwa
vyao wenyewe.
12 [h]“ ‘Ikiwa mtu atakutana kimwili na
mke wa mwanawe, lazima wote wawili
wauawe. Walichokifanya ni upotovu; damu
yao itakuwa juu ya vichwa vyao wenyewe.
13 [i]“ ‘Kama mwanaume akikutana
kimwili na mwanaume mwenzake kama
vile mwanaume afanyavyo na mwanamke,
wanaume hao wawili wamefanya lililo
chukizo sana. Lazima wauawe; nayo damu
yao itakuwa juu ya vichwa vyao wenyewe.
14 [j]“ ‘Ikiwa mwanaume ataoa binti pamoja
na mama yake, huo ni uovu. Wote watatu
ni lazima wachomwe moto, ili kwamba
pasiwepo na uovu katikati yenu.
15 [k]“ ‘Kama mwanaume akikutana kimwili
na mnyama, ni lazima auawe, na pia ni
lazima mnyama huyo auawe.
16 “ ‘Kama mwanamke atamsogelea
mnyama kukutana naye kimwili, muueni
mwanamke huyo pamoja na mnyama pia.
Lazima wauawe; damu yao itakuwa juu ya
vichwa vyao wenyewe.
17 [l]“ ‘Ikiwa mtu anamwoa dada yake, binti
aliyezaliwa na baba yake au mama yake,
nao wakakutana kimwili, ni aibu. Lazima
wakatiliwe mbali machoni pa watu wao.
Huyo mwanaume amemwaibisha dada
yake, hivyo atawajibika kwa ajili ya uovu
huo.
18 [m]“ ‘Ikiwa mwanaume atalala na
mwanamke aliye katika hedhi yake na
kukutana naye kimwili, amefunua mtiririko
wa hedhi yake, naye huyo mwanamke
amejifunua uchi wake. Wote wawili lazima
wakatiliwe mbali na watu wao.
19 “ ‘Usikutane kimwili na dada wa mama
yako wala wa baba yako, kwa maana hilo
litamwaibisha jamaa wa karibu; ninyi
wawili mtawajibika kwa ajili ya uovu huo.
20 [n]“ ‘Ikiwa mwanaume atakutana kimwili
na shangazi yake, amemwaibisha mjomba
wake. Nao watawajibika kwa ajili ya uovu
huo; watakufa bila kuzaa mtoto.
21 [o]“ ‘Ikiwa mwanaume ataoa mke
wa ndugu yake, hili ni tendo chafu;
amemwaibisha ndugu yake. Nao hawatazaa
mtoto.

---

[a]**20:5** Kut 20:5; Law 17:7
[b]**20:6** Law 19:31
[c]**20:7** Law 11:44, 45; Kut 29:1; 31:13; Efe 1:4; 1Pet 1:16; Kut 6:2; 20:2
[d]**20:8** Mwa 26:5; Kut 31:13; Eze 20:12
[e]**20:9** Kut 20:12; 21:17; Yer 35:16; Mal 1:6; 2:10; Kum 21:21; 22:30; 27:16; Eze 18:13; 22:7; 33:4-5; Mt 15:4; Mk 7:10; Yos 2:19; 2Sam 1:16; 3:29; 1Fal 2:37
[f]**20:10** Kut 20:14; 21:12; Kum 5:18; 22:22; Yn 8:5; Mwa 38:24
[g]**20:11** Law 18:7-8; Kum 27:23
[h]**20:12** Mwa 11:31; 38:16; Law 18:15
[i]**20:13** Law 18:22
[j]**20:14** Law 18:8, 17; 21:9; Hes 16:39; Amu 14:15; 15:6; Kum 27:23
[k]**20:15** Kut 20:10; 22:19; Law 18:23; 18:9; 5:1; Mwa 17:14; 20:12
[l]**20:17** Mwa 26:5; Kut 31:13; Eze 20:12; Mwa 26:5; Kut 31:13; Eze 20:12
[m]**20:18** Law 15:24; Eze 18:6; 20:19; Law 18:2, 12
[n]**20:20** Law 18:13-14; Mwa 15:2
[o]**20:21** Law 18:16; Mt 14:4; Mk 6:18

22 [a]“ ‘Zishikeni amri na sheria zangu zote
na kuzifuata, ili nchi ninayowaleta kuishi
isiwatapike. 23 [b]Kamwe msiishi kwa kufuata
desturi za mataifa nitakayoyafukuza mbele
yenu. Kwa sababu walifanya mambo
haya yote, nami nikachukizwa sana nao.
24 [c]Lakini niliwaambia ninyi, “Mtaimiliki
nchi yao; nitawapa ninyi kuwa urithi, nchi
inayotiririka maziwa na asali.” Mimi ndimi
Bwana Mungu wenu, ambaye amewatenga
kutoka mataifa.

25 [d]“ ‘Kwa hiyo, ninyi lazima mweze
kutofautisha kati ya wanyama walio safi
na wasio safi, pia kati ya ndege wasio safi
na walio safi. Msijitie unajisi kutokana
na mnyama yeyote, au ndege, wala kitu
chochote kitambaacho juu ya ardhi, vile
ambavyo nimevitenga kuwa najisi kwa ajili
yenu. 26 [e]Mtakuwa watakatifu kwangu, kwa
sababu Mimi, Bwana, ni mtakatifu, nami
nimewatenga kutoka mataifa kuwa wangu
mwenyewe.

27 [f]“ ‘Mwanaume au mwanamke ambaye
ni mchawi, mwaguzi au mwenye kupunga
pepo miongoni mwenu lazima auawe.
Mtawapiga kwa mawe; nayo damu yao
itakuwa juu ya vichwa vyao wenyewe.’ ”

*Sheria Kwa Ajili Ya Makuhani*

21 [g]Bwana akamwambia Mose, “Sema
na makuhani, wana wa Aroni,
uwaambie: ‘Kamwe kuhani asijitie unajisi
kwa utaratibu wa kiibada kwa ajili ya mtu
wake yeyote anayekufa, 2 isipokuwa jamaa
wake wa karibu, kama vile mama yake au
baba yake, mwanawe au binti yake, ndugu
yake, 3 [h]au dada yake asiyeolewa ambaye
anamtegemea kwa kuwa hana mume, kwa
ajili ya hao aweza kujitia unajisi. 4 Kamwe
asijitie unajisi mwenyewe kutokana na wale
watu ambao anahusiana nao kwa kuoana,
na hivyo kujitia unajisi.

5 “ ‘Kamwe makuhani wasinyoe nywele
za vichwa vyao wala wasinyoe pembeni
mwa ndevu zao, au kuweka chale kwenye
miili yao. 6 [i]Lazima wawe watakatifu kwa
Mungu wao, na kamwe wasilinajisi jina la
Mungu wao. Kwa sababu ndio wanaotoa
sadaka za kuteketezwa kwa moto kwa
Bwana, chakula cha Mungu wao, hivyo
lazima wawe watakatifu.

7 [j]“ ‘Kamwe wasioe wanawake
waliojinajisi kwa ukahaba, au waliopewa
talaka na waume wao, kwa sababu
makuhani ni watakatifu kwa Mungu wao.
8 Waoneni kuwa watakatifu, kwa sababu
ndio wanaotoa chakula cha Mungu wenu.
Kumbukeni kuwa ni watakatifu, kwa
sababu Mimi Bwana ni mtakatifu, Mimi
niwafanyaye ninyi kuwa watakatifu.

9 “ ‘Ikiwa binti wa kuhani anajitia unajisi
kwa kufanya ukahaba, anamwaibisha baba
yake; lazima achomwe kwa moto.

10 [k]“ ‘Kuhani mkuu, yule miongoni mwa
ndugu zake ambaye amekwisha kutiwa
mafuta kwa kumiminiwa juu ya kichwa
chake, na ambaye amewekwa wakfu kuvaa
mavazi ya ukuhani, kamwe asiache nywele
zake bila kufunikwa, wala asirarue nguo
zake. 11 [l]Kamwe asiingie mahali palipo
maiti ndani. Kamwe asijitie unajisi, hata
kwa ajili ya baba yake au mama yake,
12 [m]wala asiondoke mahali patakatifu pa
Mungu wake au kupanajisi, kwa sababu
amewekwa wakfu kwa mafuta ya Mungu
wake. Mimi ndimi Bwana.

[a]**20:22** Mwa 26:5; Law 18:25-28
[b]**20:23** Law 18:3, 24-25, 27-30
[c]**20:24** Kut 3:8; 13:5; 33:16; Hes 14:8; 16:14; 1Fal 8:53; Za 135
[d]**20:25** Law 10:10; Kum 14:3-21; Mdo 10:14; Law 11:47
[e]**20:26** Kum 14:2; Law 19:2; Yos 24:19; 2Fal 19:22
[f]**20:27** Kut 22:18; Law 19:31; 24:14; Kum 18:10; 1Sam 28:7
[g]**21:1** Kut 28:1; Law 5:3; 13:3; Hes 5:2; 6:6; 19:11; 31:19; Eze 44:25
[h]**21:3** Hes 6:6; 21:5; Law 13:40; 19:28; Yer 7:29; 16:6; Eze 5:1; 44:20
[i]**21:6** Ezr 8:28; Law 18:21; 3:11; 22:25; 10:3; Kut 19:22; Law 20:7; Za 15:4; Mt 5:33-37; Yak 5:12
[j]**21:7** Eze 44:22; 21:8; Law 3:11; Kut 31:13; 21:9; Mwa 38:24; Law 19:29; Kut 29:29; Hes 35:25; Kut 28:2
[k]**21:10** Kut 29:7; Law 8:7-13; 16:4; 10:6
[l]**21:11** Hes 5:2; 6:6; 9:6; 19:11-14; 31:19; Law 19:28
[m]**21:12** Kut 25:8; 28:41; Law 10:7

13 [a]“ ‘Mwanamke kuhani atakayemwoa
lazima awe bikira. 14 Kamwe asimwoe
mjane, au mwanamke aliyepewa talaka,
wala mwanamke aliyejinajisi kwa ukahaba,
bali atamwoa tu bikira kutoka miongoni
mwa watu wake, 15 [b]na hivyo hatawatia
unajisi watoto wake miongoni mwa watu
wake. Mimi ndimi Bwana, nimfanyaye
mtakatifu.’ ”
16 Bwana akamwambia Mose,
17 [c]“Mwambie Aroni: ‘Kwa vizazi vijavyo,
hakuna mzao wako mwenye dosari
atakayekaribia kutoa chakula cha Mungu
wake. 18 [d]Hakuna mtu mwenye dosari yoyote
awezaye kukaribia: hakuna mtu aliye kipofu
au kiwete, au aliyeharibika uso au asiye
na viungo kamili, 19 hakuna mtu mwenye
mguu au mkono uliolemaa, 20 [e]au mwenye
kibiongo au aliyedumaa, au aliye na tatizo
la macho, au aliye na uvimbe wenye usaha
au majipu, au aliyehasiwa. 21 [f]Hakuna mzao
wa kuhani Aroni mwenye kilema chochote
atakayekaribia kutoa sadaka kwa Bwana
ya kuteketezwa kwa moto. Kama ana
kilema, kamwe asikaribie kutoa chakula
cha Mungu wake. 22 [g]Anaweza kula chakula
kitakatifu sana cha Mungu wake, pia hata
chakula kitakatifu. 23 [h]Lakini kwa sababu
ya kilema chake, kamwe asikaribie karibu
na pazia wala kukaribia madhabahu, asije
akanajisi mahali patakatifu pangu. Mimi
ndimi Bwana, niwafanyaye watakatifu.’ ”
24 Basi Mose akamwambia Aroni jambo
hili na wanawe, pamoja na Waisraeli wote.

*Matumizi Ya Sadaka Takatifu*

22 Bwana akamwambia Mose,
2 [i]“Mwambie Aroni na wanawe
kushughulikia kwa uangalifu sadaka
takatifu Waisraeli wanazoziweka wakfu
kwangu, ili wasilinajisi Jina langu takatifu.
Mimi ndimi Bwana.
3 [j]“Waambie: ‘Katika vizazi vijavyo,
ikiwa yeyote wa wazao wako ni najisi kwa
taratibu za kiibada, naye akakaribia sadaka
takatifu zile Waisraeli wanazoweka wakfu
kwa Bwana, mtu huyo lazima akatiliwe
mbali na uso wangu. Mimi ndimi Bwana.
4 [k]“ ‘Ikiwa mzao wa Aroni ana ugonjwa wa
ngozi unaoambukiza au anatokwa na usaha
mwilini, hawezi kula sadaka takatifu mpaka
atakasike. Pia atakuwa najisi ikiwa atagusa
kitu chochote kilicho najisi kwa kugusa
maiti au mtu aliyetokwa na shahawa, 5 [l]au
ikiwa atagusa kitu chochote kitambaacho
kimfanyacho mtu najisi, au mtu yeyote
awezaye kumtia unajisi, hata unajisi uwe
gani. 6 [m]Mtu anayegusa kitu chochote cha
aina hiyo atakuwa najisi mpaka jioni.
Kamwe hatakula sadaka yoyote takatifu
mpaka yeye mwenyewe awe ameoga kwa
maji. 7 [n]Wakati jua linapotua, atakuwa safi,
na baadaye anaweza kula sadaka takatifu,
kwa kuwa ni vyakula vyake. 8 [o]Kamwe
asile nyama ya mzoga wala iliyoraruliwa
na wanyama pori, naye akatiwa unajisi kwa
hilo. Mimi ndimi Bwana.
9 [p]“ ‘Makuhani lazima washike maagizo
yangu ili wasiwe na hatia, wakafa
kwa kuyadharau. Mimi ndimi Bwana
ninayewafanya watakatifu.
10 [q]“ ‘Hakuna mtu yeyote asiye wa jamaa ya
kuhani anayeruhusiwa kula sadaka takatifu,
hata mgeni wa kuhani au mfanyakazi
wake haruhusiwi kuila. 11 [r]Lakini ikiwa
kuhani amenunua mtumwa kwa fedha,
au mtumwa amezaliwa katika nyumba ya

---

[a]**21:13** Eze 44:22
[b]**21:15** Rum 12:1; 1Kor 3:16; Efe 5:17; 1The 4:1-8
[c]**21:17** Hes 16:5; Za 64:4
[d]**21:18** Law 22:19-25; 19:14; 2Sam 4:4; 9:3; 19:26
[e]**21:20** Law 22:24; Kum 23:1; Isa 56:3
[f]**21:21** Law 3:11; 22:19
[g]**21:22** 1Kor 9:13
[h]**21:23** Kut 25:8; Law 20:8; Hes 18:19
[i]**22:2** Law 19:8; Kut 20:7; Mt 5:33; Eze 44:8; Hes 15:15, 31; Kut 28:38; Kum 15:19
[j]**22:3** Ezr 8:28; Law 7:20-21; Hes 19:13
[k]**22:4** Law 14:1-32; 15:2-15; 11:24-28, 39; Hes 19:11
[l]**22:5** Law 11:24-28, 43; 15:7
[m]**22:6** Hag 2:13; Law 11:24; 14:8; Ebr 10:22
[n]**22:7** Hes 18:11
[o]**22:8** Law 11:39-44; 17:15; Kut 22:31
[p]**22:9** Law 8:35; 20:8; Kut 28:38-43; Hes 18:22
[q]**22:10** Kut 12:45; 29:33; Hes 3:10; 1Sam 21:6
[r]**22:11** Mwa 17:13; Kut 12:44

kuhani huyo, mtumwa huyo aweza kula chakula cha huyo kuhani. [12] Ikiwa binti wa kuhani ameolewa na mtu asiye kuhani, binti huyo haruhusiwi kula chochote cha matoleo matakatifu. [13] Lakini ikiwa binti wa kuhani amekuwa mjane au amepewa talaka, naye hana watoto, na akarudi kuishi na jamaa ya baba yake kama wakati wa usichana wake, binti huyo anaweza kula chakula cha baba yake. Hata hivyo, mtu asiyeruhusiwa hawezi kula chochote katika chakula hiki.

[14] [a]" 'Ikiwa mtu yeyote amekula sadaka takatifu kwa makosa, lazima atoe malipo ya sadaka hiyo kwa kuhani na kuongeza sehemu ya tano ya thamani ya sadaka hiyo. [15] [b]Kamwe makuhani wasiinajisi sadaka takatifu ambayo Waisraeli wameitoa kwa BWANA [16] [c]kwa kuwaruhusu kuzila sadaka hizo takatifu, na hivyo kuwaletea hatia ya kudaiwa malipo. Mimi ndimi BWANA niwafanyaye watakatifu.' "

*Dhabihu Zisizokubalika*

[17] BWANA akamwambia Mose, [18] [d]"Sema na Aroni na wanawe, na Waisraeli wote uwaambie: 'Ikiwa mmoja wenu, aliye Mwisraeli au mgeni anayeishi katika nchi ya Israeli, atatoa matoleo kwa ajili ya sadaka ya kuteketezwa kwa moto kwa BWANA, iwe kutimiza nadhiri au kuwa sadaka ya hiari, [19] [e]lazima mtoe mnyama dume asiye na dosari, akiwa ng'ombe, mbuzi au kondoo, ili aweze kukubalika kwa niaba yako. [20] [f]Kamwe usitoe kitu chochote chenye dosari kwa sababu hakitakubaliwa kwa niaba yako. [21] [g]Mtu yeyote aletapo sadaka ya amani kwa BWANA kutoka kundi la ng'ombe au mbuzi ili kutimiza nadhiri maalum au sadaka ya hiari, lazima sadaka hiyo isiwe na dosari au waa ili ikubalike. [22] Kamwe usimtolee BWANA mnyama aliye kipofu, aliyejeruhiwa wala aliye kilema, au chochote kilicho na uvimbe, au chenye upele au vidonda vinavyotoka usaha. Kamwe chochote cha aina hii kisiwekwe juu ya madhabahu kuwa sadaka iliyotolewa kwa BWANA ya kuteketezwa kwa moto. [23] [h]Lakini waweza ukatoa ng'ombe au kondoo mwenye kilema au aliyedumaa kama sadaka ya hiari, lakini hii haitakubalika kuwa sadaka ya kutimiza nadhiri. [24] [i]Kamwe usimtolee BWANA mnyama ambaye mapumbu yake yamejeruhiwa, au kuhasiwa, au kuraruliwa au kukatwa. Kamwe usifanye hivi katika nchi yako mwenyewe, [25] [j]na kamwe usikubali wanyama wa aina hii kutoka mkono wa mgeni ili kuwatoa wanyama hao kuwa chakula kwa Mungu wako. Wanyama hao hawatakubaliwa kwa niaba yako, kwa sababu wana vilema, nao wana dosari.' "

[26] BWANA akamwambia Mose, [27] [k]"Wakati ndama, mwana-kondoo au mwana-mbuzi azaliwapo, atabaki na mama yake kwa siku saba. Kuanzia siku ya nane na kuendelea anaweza kukubaliwa kuwa sadaka iliyotolewa kwa BWANA kwa kuteketezwa kwa moto. [28] [l]Usimchinje ng'ombe na ndama wake, au kondoo na kitoto chake siku moja.

[29] [m]"Unapomtolea BWANA dhabihu ya shukrani, itoe kwa namna ambayo itakubalika kwa niaba yako. [30] [n]Ni lazima iliwe siku iyo hiyo, pasipo kubakiza chochote mpaka asubuhi. Mimi ndimi BWANA.

[31] [o]"Shikeni maagizo yangu na kuyafuata. Mimi ndimi BWANA. [32] [p]Msilinajisi Jina

[a]**22:14** Law 4:2; 5:15
[b]**22:15** Law 19:8; Hes 18:32
[c]**22:16** Hes 18:11; Kut 28:38; Law 20:8
[d]**22:18** Hes 15:8, 16; 19:10; Yos 8:33; Mwa 28:20; Za 22:25; 76:11; 116:8; Law 7:16
[e]**22:19** Law 1:2; 21:18-21; Hes 28:11; Kum 15:21
[f]**22:20** Kum 15:21; 17:1; Eze 43:23; 45:18; 46:6; Mal 1:8; Ebr 9:14; 1Pet 1:19; Kut 28:38
[g]**22:21** Kut 12:5; 32:6; Law 3:6; 7:16; Mal 1:14; Amo 4:5; Hes 15:38
[h]**22:23** Law 21:18
[i]**22:24** Law 21:20
[j]**22:25** Law 21:6; 1:3; 3:1; Hes 19:2; 15:15
[k]**22:27** Law 1:3; Kut 22:30; 28:38
[l]**22:28** Kum 22:6-7
[m]**22:29** Law 7:12; Za 107:22
[n]**22:30** Law 7:15; 11:44; Za 116:17
[o]**22:31** Kum 4:2; Za 105:45; Kut 22:31; Law 19:37; Hes 15:40
[p]**22:32** Law 18:21; 10:3; 20:8

langu takatifu. Lazima nikubalike kuwa mtakatifu kwa Waisraeli. Mimi ndimi BWANA ninayewafanya watakatifu, 33 [a]na niliyewatoa katika nchi ya Misri niwe Mungu wenu. Mimi ndimi BWANA."

*Sikukuu Zilizoamriwa*

23 BWANA akamwambia Mose, 2 [b]"Sema na Waisraeli na uwaambie: 'Hizi ndizo sikukuu zangu zilizoamriwa, sikukuu zilizoamriwa za BWANA, ambazo mtazitangaza kuwa makusanyiko matakatifu.

*Sabato*

3 [c]" 'Kuna siku sita mnazoweza kufanya kazi, lakini siku ya saba ni Sabato ya kupumzika, siku ya kusanyiko takatifu. Hamtafanya kazi yoyote. Popote mnapoishi, ni Sabato kwa BWANA.

*Pasaka Na Mikate Isiyotiwa Chachu*

**(Hesabu 28:16-25)**

4 [d]" 'Hizi ni sikukuu za BWANA zilizoamriwa, makusanyiko matakatifu mtakayoyatangaza kwa nyakati zilizoamriwa: 5 [e]Pasaka ya BWANA huanza jioni ya siku ya kumi na nne ya mwezi wa kwanza. 6 [f]Siku ya kumi na tano ya mwezi huo wa kwanza, Sikukuu ya BWANA ya Mikate Isiyotiwa Chachu huanza; kwa siku saba, mtakula mikate isiyotiwa chachu.
7 Katika siku ya kwanza, mtakuwa na kusanyiko takatifu, na msifanye kazi zenu za kawaida. 8 Kwa siku saba mtamletea BWANA sadaka ya kuteketezwa kwa moto. Kwenye siku hiyo ya saba mtafanya kusanyiko takatifu, na msifanye kazi zenu za kawaida.' "

*Malimbuko*

9 BWANA akamwambia Mose, 10 [g]"Sema na Waisraeli na uwaambie: 'Mtakapoingia katika nchi nitakayowapa na kuvuna mazao ya nchi hiyo, leteni kwa kuhani mganda wa nafaka ya kwanza mtakayovuna. 11 [h]Naye atauinua huo mganda mbele za BWANA ili ukubaliwe kwa niaba yenu; kuhani ataupunga siku inayofuata Sabato. 12 [i]Siku hiyo mtakapoinua huo mganda, lazima mtoe kwa BWANA dhabihu ya kuteketezwa kwa moto ya mwana-kondoo wa mwaka mmoja asiye na dosari, 13 [j]pamoja na sadaka yake ya nafaka ya sehemu mbili za kumi za efa[k] za unga laini uliochanganywa na mafuta, sadaka iliyotolewa kwa BWANA kwa kuteketezwa kwa moto, harufu nzuri ya kupendeza, na sadaka yake ya kinywaji ya robo ya hini[l] ya divai. 14 [m]Kamwe msile mkate wowote, au nafaka iliyokaangwa au nafaka mpya, mpaka siku ile mtakayomletea Mungu wenu sadaka hii. Hili litakuwa agizo la kudumu kwa vizazi vijavyo, popote mnapoishi.

*Sikukuu Ya Majuma*

**(Hesabu 28:26-31)**

15 " 'Tangu siku ile iliyofuata Sabato, siku mliyotoa sadaka ya mganda wa kuinuliwa, hesabuni majuma saba kamili. 16 [n]Mtahesabu siku hamsini mpaka siku inayofuata Sabato ya saba, ndipo mtatoa sadaka ya nafaka mpya kwa BWANA. 17 [o]Kutoka popote mnapoishi, mtaleta mikate miwili ya unga laini, sehemu mbili za kumi za efa, uliookwa kwa chachu, kuwa sadaka ya kuinuliwa ya

[a]**22:33** Kut 6:6; Mwa 17:7; Law 11:45
[b]**23:2** Hes 29:39; Eze 44:24; Kol 2:16; Isa 6:3; Mt 6:9; Yn 12:28; Kut 32:5; Hes 10:2-3; 2Nya 30:5
[c]**23:3** Kut 20:9-10; Ebr 4:9-10; Kum 5:13; Hes 28:26; Lk 13:14; Neh 13:22; Isa 56:2; 58:13
[d]**23:4** Nah 1:15; Kut 23:14
[e]**23:5** Kut 12:6-11; Hes 28:16-17; Kum 16:1-8; Yos 5:10
[f]**23:6** Kut 12:17-19
[g]**23:10** Hes 15:2; Law 19:9; Kut 22:29; 34:22; Rum 11:16; Kum 16:9; Yos 3:15; Mit 3:9; 1Kor 15:20; Yak 1:18
[h]**23:11** Kut 29:24; 28:38; Law 9:21; 10:14
[i]**23:12** Law 12:6; Kut 12:5
[j]**23:13** Law 2:14-16; 6:20; 10:9; 24:5; Hes 15:6; 28:9; Mwa 35:14
[k]13 Sehemu mbili za kumi za efa ni sawa na kilo mbili.
[l]13 Robo ya hini ni sawa na lita moja.
[m]**23:14** Yos 5:11; Rut 2:14; 1Sam 17:17; 25:18; 2Sam 17:28; Kut 34:26; Law 3:17; Hes 10:8; 15:21; Yer 2:3
[n]**23:16** Mdo 20:16; 2:1; Hes 28:26
[o]**23:17** Kut 34:22; 23:16; Hes 15:17-19

malimbuko kwa BWANA. 18 [a]Toeni pamoja
na hiyo mikate wana-kondoo saba, kila
mmoja wa mwaka mmoja asiye na dosari,
na fahali mchanga, na kondoo dume wawili.
Watakuwa sadaka ya kuteketezwa kwa
moto iliyotolewa kwa BWANA, pamoja na
sadaka za nafaka na sadaka za vinywaji,
sadaka iliyotolewa kwa moto yenye harufu
nzuri ya kumpendeza BWANA. 19 [b]Kisha
toeni dhabihu ya mbuzi dume mmoja kwa
ajili ya sadaka ya dhambi, na wana-kondoo
wawili, kila mmoja wa mwaka mmoja,
kwa ajili ya sadaka ya amani. 20 [c]Kuhani
atawainua hao wana-kondoo wawili mbele
za BWANA kuwa sadaka ya kuinuliwa,
pamoja na mkate wa malimbuko. Ni sadaka
takatifu kwa BWANA kwa ajili ya kuhani.
21 [d]Siku iyo hiyo mtatangaza kusanyiko
takatifu, na msifanye kazi zenu za kawaida.
Hili litakuwa agizo la kudumu kwa vizazi
vijavyo, popote mnapoishi.

22 [e]" 'Mnapovuna mavuno ya ardhi yenu,
msivune hadi mpakani mwa shamba lenu,
au kukusanya masazo ya mavuno yenu.
Hayo utayaacha kwa ajili ya maskini na
mgeni. Mimi ndimi BWANA Mungu wenu.' "

*Sikukuu Ya Tarumbeta*

### (Hesabu 29:1-6)

23 BWANA akamwambia Mose,
24 [f]"Waambie Waisraeli: 'Katika siku ya
kwanza ya mwezi wa saba mtakuwa na
siku ya mapumziko, kusanyiko takatifu
la ukumbusho litakaloadhimishwa kwa
kupiga tarumbeta. 25 Msifanye kazi zenu
zozote za kawaida, lakini toeni sadaka kwa
BWANA iliyoteketezwa kwa moto.' "

*Siku Ya Upatanisho*

### (Hesabu 29:7-11)

26 BWANA akamwambia Mose, 27 [g]"Siku
ya kumi ya mwezi huu wa saba ni Siku ya
Upatanisho. Mtafanya kusanyiko takatifu,
mfunge, nanyi mtoe sadaka kwa BWANA
ya kuteketezwa kwa moto. 28 Msifanye
kazi siku hiyo, kwa sababu ni Siku ya
Upatanisho, ambapo upatanisho unafanyika
kwa ajili yenu mbele za BWANA Mungu
wenu. 29 [h]Mtu yeyote ambaye hatafunga
siku hiyo ni lazima akatiliwe mbali na
watu wake. 30 [i]Mtu yeyote atakayefanya
kazi siku hiyo nitamwangamiza kutoka
miongoni mwa watu wake. 31 [j]Hamtafanya
kazi kamwe. Hili litakuwa agizo la kudumu
kwa vizazi vijavyo popote mnapoishi. 32 [k]Ni
Sabato ya mapumziko kwenu ninyi, na
lazima mfunge. Tangu jioni ya siku ya tisa
ya mwezi hadi jioni inayofuata, mtaishika
Sabato yenu."

*Sikukuu Ya Vibanda*

### (Hesabu 29:12-40)

33 BWANA akamwambia Mose,
34 [l]"Waambie Waisraeli: 'Katika siku ya
kumi na tano ya mwezi wa saba, Sikukuu
ya BWANA ya vibanda itaanza, nayo
itaadhimishwa kwa siku saba. 35 Siku ya
kwanza ni kusanyiko takatifu, msifanye
kazi zenu za kawaida. 36 [m]Kwa siku saba
toeni sadaka kwa BWANA za kuteketezwa
kwa moto. Kwenye siku ya nane fanyeni
kusanyiko takatifu, na mtoe sadaka kwa
BWANA ya kuteketezwa kwa moto. Ni
kusanyiko la mwisho, msifanye kazi zenu
za kawaida.

37 (" 'Hizi ni sikukuu za BWANA
zilizoamriwa, ambazo mtazitangaza kuwa
makusanyiko matakatifu kwa kuleta sadaka

---

[a]**23:18** Kut 29:41; 30:9; 37:16; Yer 19:13; 44:18
[b]**23:19** Hes 28:30; Law 4:23
[c]**23:20** Kut 29:24
[d]**23:21** Kut 32:5
[e]**23:22** Law 19:9-10; Kum 24:19-21; Rut 2:2, 15; Kut 23:11; Kum 15:1-18; Ay 20:19; Za 112:9; Mit 14:31; Isa 58:7-8; Yak 2:1
[f]**23:24** Ezr 3:1; Hes 10:9-10; 29:1; 31:6; 2Fal 11:14; 2Nya 13:12; Za 98:6
[g]**23:27** Law 16:29; Kut 30:10; Hes 29:7; Isa 58:3-5; Dan 10:3, 12
[h]**23:29** Mwa 17:14; Law 7:20; Hes 5:2
[i]**23:30** Law 20:3
[j]**23:31** Law 3:17
[k]**23:32** Law 16:31; Neh 13:19
[l]**23:34** 1Fal 8:2; Hag 2:1; Kut 23:16; Yn 7:2, 37; Kut 34:22; Ezr 3:4; Neh 8:14; Zek 14:16
[m]**23:36** 1Fal 8:2; 2Nya 7:9; Neh 8:18; Yn 7:37; Law 1:9

kwa BWANA za kuteketeza kwa moto:
sadaka za kuteketezwa na sadaka za nafaka,
dhabihu na sadaka za vinywaji zitahitajika
kila siku. 38 [a]Sadaka hizi ni nyongeza ya zile
mnazozitoa katika Sabato za BWANA, na pia
ni nyongeza ya matoleo yenu ya chochote
mlichoweka nadhiri, na sadaka zenu zote
za hiari mnazozitoa kwa BWANA.)

39 [b]“ ‘Basi kuanzia siku ya kumi na tano
ya mwezi wa saba, baada ya kuvuna mazao
yote ya nchi, mtaadhimisha sikukuu kwa
BWANA kwa siku saba; siku ya kwanza ni
mapumziko, pia siku ya nane ni mapumziko.
40 [c]Siku ya kwanza mtachukua matunda
mazuri ya miti, matawi ya mitende, matawi
yenye majani mengi, na matawi ya mirebi,
nanyi mtashangilia mbele za BWANA Mungu
wenu kwa siku saba. 41 Mtaadhimisha siku
hii kuwa sikukuu kwa BWANA kwa siku
saba kila mwaka. Hili litakuwa agizo la
kudumu kwa vizazi vijavyo; iadhimisheni
mwezi wa saba. 42 [d]Mtaishi katika vibanda
kwa siku saba: Wazawa wote wa Waisraeli
wataishi katika vibanda, 43 [e]ili wazao wenu
wajue kuwa niliwafanya Waisraeli waishi
kwenye vibanda nilipowatoa Misri. Mimi
ndimi BWANA Mungu wenu.’ ”

44 Kwa hiyo Mose akawatangazia
Waisraeli sikukuu zilizoamriwa na BWANA.

### *Mafuta Na Mikate Mbele Za BWANA*

24 BWANA akamwambia Mose,
2 [f]“Waagize Waisraeli wakuletee
mafuta safi ya zeituni yaliyokamuliwa
kwa ajili ya mwanga ili taa ziwe zinawaka
daima. 3 [g]Nje ya pazia la Ushuhuda ndani
ya Hema la Kukutania, Aroni ataziwasha
taa mbele za BWANA kuanzia jioni hadi
asubuhi bila kuzima. Hili litakuwa agizo
la kudumu kwa vizazi vijavyo. 4 [h]Taa zilizo
juu ya kinara cha dhahabu safi mbele za
BWANA lazima zihudumiwe daima.

5 [i]“Chukua unga laini, uoke mikate kumi
na miwili, ukitumia sehemu mbili za kumi
za efa[j] za unga kwa kila mkate. 6 [k]Iweke
katika mistari miwili, kila mstari mikate
sita, uiweke mbele za BWANA juu ya meza
iliyotengenezwa kwa dhahabu safi. 7 [l]Kando
ya kila mstari, weka uvumba safi kama
sehemu ya kumbukumbu ili kuwakilisha
mikate kuwa sadaka iliyotolewa kwa
BWANA kwa kuteketezwa kwa moto.
8 [m]Mikate hii itawekwa mbele za BWANA
kila wakati, Sabato baada ya Sabato,
kwa niaba ya Waisraeli, kuwa Agano la
kudumu. 9 [n]Hii ni mali ya Aroni na wanawe,
watakaoila katika mahali patakatifu, kwa
sababu ni sehemu takatifu sana ya fungu
lao la kawaida la sadaka iliyotolewa kwa
BWANA kwa kuteketezwa kwa moto.”

### *Mwenye Kukufuru Apigwa Mawe*

10 Basi mwana wa mama Mwisraeli na
baba Mmisri alikwenda miongoni mwa
Waisraeli, nayo mapigano yakatokea
ndani ya kambi kati yake na Mwisraeli.
11 [o]Huyu mwana wa mwanamke Mwisraeli
akalikufuru Jina la BWANA kwa kulaani;
kwa hiyo wakamleta kwa Mose. (Jina
la mama yake aliitwa Shelomithi binti
wa Dibri, wa kabila la Dani.) 12 [p]Nao
wakamweka mahabusu mpaka mapenzi
ya BWANA yawe wazi kwao.

13 Ndipo BWANA akamwambia Mose:

[a]**23:38** Kut 20:10; 2Nya 2:4; Eze 45:17; Law 7:16
[b]**23:39** Isa 62:9; Kut 23:16; Kum 16:13; Mt 21:8
[c]**23:40** Za 9:2; 66:6; 105:43; 118:27; 137:2; Neh 8:10, 14-17; Isa 44:4; Kum 12:7; 14:26; 28:47; Yoe 2:26
[d]**23:42** Kut 23:16; Neh 8:14-16
[e]**23:43** Kum 31:13; Za 78:5
[f]**24:2** Kut 27:20; 39:37; Hes 8:2-4
[g]**24:3** Kut 12:14
[h]**24:4** Kut 25:31; 31:8
[i]**24:5** Kut 25:30; Ebr 9:2; Law 23:13; Kut 40:24
[j]5 Sehemu mbili za kumi za efa ni sawa na kilo mbili.
[k]**24:6** Kut 25:23-30; Hes 4:7; 1Fal 7:48; Ebr 9:2; 1Nya 9:32
[l]**24:7** Law 2:1-2
[m]**24:8** Kut 25:30; 1Nya 9:32; 2Nya 2:2-4; Mt 12:5
[n]**24:9** Law 6:16-17; 8:31; Mt 12:4; Mk 2:26; Lk 6:4; 1Sam 9:21; Kut 29:33
[o]**24:11** Kut 3:15; 18:22; 20:7; 31:2; 2Fal 6:33; Ay 1:11; Hes 1:4; 7:2; 10:15; 13:2; 17:2; Yos 7:18; 1Fal 7:18
[p]**24:12** Kut 18:16; Hes 15:34

14 [a]“Mchukue huyo aliyekufuru nje ya
kambi. Wale wote waliomsikia akikufuru
wataweka mikono juu ya kichwa chake,
kisha kusanyiko lote litampiga mawe.
15 [b]Waambie Waisraeli: ‘Ikiwa mtu yeyote
atamlaani Mungu wake, atakuwa na hatia
kwa uovu wake; 16 [c]yeyote atakayekufuru
Jina la BWANA ni lazima auawe. Kusanyiko
lote litampiga kwa mawe. Iwe ni mgeni au
mzawa, atakapolikufuru Jina la BWANA, ni
lazima auawe.

17 [d]“ ‘Kama mtu yeyote atamuua mtu
mwingine, ni lazima auawe. 18 Mtu
yeyote auaye mnyama wa mtu mwingine
lazima afidie, uhai kwa uhai. 19 Ikiwa mtu
yeyote atamjeruhi jirani yake, chochote
alichomtenda naye atatendewa: 20 [e]iwapo
amemvunja mfupa atavunjwa mfupa,
jicho kwa jicho, jino kwa jino. Kama
alivyomjeruhi mwenzake, vivyo hivyo
ndivyo atakavyojeruhiwa. 21 [f]Yeyote
auaye mnyama wa mtu lazima alipe fidia,
lakini yeyote auaye mtu, lazima auawe.
22 [g]Mtakuwa na sheria iyo hiyo kwa mgeni
na kwa mzawa. Mimi ndimi BWANA Mungu
wenu.’ ”

23 [h]Kisha Mose akasema na Waisraeli,
nao wakamchukua yule aliyekufuru nje
ya kambi na kumpiga mawe. Waisraeli
wakafanya kama BWANA alivyomwagiza
Mose.

*Mwaka Wa Sabato*

**(Kumbukumbu 15:1-11)**

25 [i]BWANA akamwambia Mose katika
Mlima Sinai, 2 [j]“Sema na Waisraeli
uwaambie: ‘Mtakapoingia katika nchi
ninayowapa ninyi, nchi yenyewe ni
lazima ishike Sabato kwa ajili ya BWANA.
3 [k]Kwa miaka sita mtapanda mazao katika
mashamba yenu, nanyi kwa miaka sita
mtaikata mizabibu yenu matawi na kuvuna
mazao yake. 4 [l]Lakini mwaka wa saba nchi
lazima iwe na Sabato ya mapumziko, Sabato
kwa BWANA. Msipande mbegu katika
mashamba yenu, wala msikate mizabibu
yenu matawi. 5 [m]Msivune na kuweka akiba
kinachoota chenyewe, wala kuvuna na
kusindika zabibu ambayo hamkuhudumia
mashamba yake. Nchi lazima iwe na mwaka
wa mapumziko. 6 Chochote nchi itoacho
katika mwaka wa Sabato kitakuwa chakula
chenu wenyewe, watumishi wenu wa kiume
na wa kike, mfanyakazi aliyeajiriwa, na
mkazi wa muda anayeishi miongoni
mwenu, 7 [n]vilevile malisho ya mifugo
yenu na wanyama pori katika nchi yenu.
Chochote nchi itakachozalisha kinaweza
kuliwa.

*Mwaka Wa Yubile*

8 “ ‘Hesabu Sabato saba za miaka, yaani
miaka saba mara saba, ili Sabato saba za
miaka utakuwa muda wa miaka arobaini
na tisa. 9 [o]Ndipo tarumbeta itapigwa kila
mahali katika siku ya kumi ya mwezi wa
saba. Katika Siku ya Upatanisho, piga
tarumbeta katika nchi yako yote. 10 [p]Mwaka
wa hamsini mtauweka wakfu na kutangaza
uhuru katika nchi kwa wakazi wake wote.
Itakuwa ni yubile[q] kwenu; kila mmoja wenu

[a]**24:14** Law 20:2; Kum 13:9; 17:5-7; Mdo 7:58
[b]**24:15** Kut 22:28; Law 5:1; Hes 9:13
[c]**24:16** Kut 22:28; 21:21; 1Fal 21:10-13; Mt 26:66; Mk 14:64; Yn 10:33; Mdo 7:58; Za 74:10, 18
[d]**24:17** Mwa 9:6; Kut 21:12; Kum 27:24; Hes 35:31; Mt 26:52; Ufu 13:10
[e]**24:20** Kut 21:24; Mt 5:38; Law 19:34; Kum 10:17-19
[f]**24:21** Kut 21:33
[g]**24:22** Kut 12:49; 22:21; Eze 47:22; Hes 9:14; 15:16
[h]**24:23** Kum 13:9; 17:7
[i]**25:1** Kut 19:11
[j]**25:2** Kut 23:10; Law 26:34-35; 2Nya 36:21
[k]**25:3** Kut 23:10; 25:4
[l]**25:4** Law 26:35; 2Nya 36:21; Isa 36:16; 37:30
[m]**25:5** 2Fal 19:29; Mwa 40:10; Hes 6:3; 13:20; Kum 23:24; Neh 13:15; Isa 5:2; 37:30
[n]**25:7** Kut 23:11
[o]**25:9** Law 16:29; 23:24; Hes 10:8; Yos 6:4; Amu 3:27; 7:16; 1Sam 13:3; Isa 27:13; Zek 9:14; Kut 30:10
[p]**25:10** Isa 61:1; Yer 34:8, 15, 17; Lk 4:19; Law 27:17, 21; Hes 36:4; Eze 46:17; Kut 20:2; Ezr 6:3; Gal 5:1
[q]10 Yubile ni baragumu iliopigwa kila mwaka wa hamsini; ni Sabato ya nchi ya kila mwaka wa hamsini uliokuwa mwaka wa ukombozi, yaani kuachia huru.

atairudia mali ya jamaa yake, na kila mmoja
kurudi kwenye ukoo wake. 11 Mwaka wa
hamsini utakuwa yubile kwenu, msipande
wala msivune kile kiotacho chenyewe, au
kuvuna zabibu zisizohudumiwa. 12 Kwa
kuwa ni yubile, nayo itakuwa takatifu
kwenu; mtakula tu kile kilichotoka moja
kwa moja mashambani.
13 “ ‘Katika huu Mwaka wa Yubile,
kila mmoja atarudi kwenye mali yake
mwenyewe.
14 [a]“ ‘Ikiwa utauza ardhi kwa mmoja
wa wazawa wa nchi yako, au ukinunua
ardhi kutoka kwake, mmoja asimpunje
mwingine. 15 [b]Utanunua ardhi kwa mzawa
wa nchi yako kwa misingi ya hesabu ya
miaka baada ya Yubile. Naye ataiuza kwako
kwa misingi ya hesabu ya miaka iliyobaki
kwa kuvuna mavuno. 16 Miaka inapokuwa
mingi, utaongeza bei, nayo miaka ikiwa
michache, utapunguza bei, kwa sababu
kile anachokuuzia kwa hakika ni hesabu
ya mazao. 17 [c]Mmoja asimpunje mwingine,
bali utamcha Mungu wako. Mimi ndimi
BWANA Mungu wako.
18 [d]“ ‘Fuateni amri zangu, mwe waangalifu
kutii amri zangu, nanyi mtaishi salama
katika nchi. 19 [e]Kisha nchi itazaa matunda
yake, nanyi mtakula na kushiba na kuishi
humo kwa salama. 20 Mwaweza kuuliza,
“Tutakula nini katika mwaka wa saba ikiwa
hatutapanda wala kuvuna mazao yetu?”
21 [f]Nitawapelekeeni baraka ya pekee katika
mwaka wa sita, kwamba nchi itazalisha
mazao ya kutosha kwa miaka mitatu.
22 [g]Mnapopanda mwaka wa nane, mtakula
mavuno ya miaka iliyopita. Pia mtaendelea
kuyala mazao hayo hadi mvune mavuno ya
mwaka wa tisa.
23 [h]“ ‘Kamwe ardhi isiuzwe kwa mkataba
wa kudumu, kwa sababu nchi ni mali
yangu, nanyi ni wageni na wapangaji
wangu. 24 [i]Katika nchi yote mtakayoshika
kuwa milki yenu, ni lazima mtoe ukombozi
wa ardhi.
25 [j]“ ‘Ikiwa mmoja wa wazawa wa nchi
yako amekuwa maskini na akauza baadhi
ya mali yake, ndugu yake wa karibu atakuja
na kukomboa kile ndugu yako alichokiuza.
26 Iwapo mtu huyo hana jamaa wa karibu wa
kukomboa mali hiyo kwa ajili yake, lakini
yeye mwenyewe akafanikiwa na kupata
mali itoshayo kuikomboa, 27 ataamua tena
thamani yake kwa miaka tangu alipoiuza,
na kurudisha kiasi kilichobaki cha thamani
kwa mtu ambaye alikuwa amemuuzia
mali hiyo, naye ataweza kuirudia mali
yake. 28 Lakini kama hatapata njia ya
kumlipa mnunuzi, ile mali aliyouza itabaki
kumilikiwa na mnunuzi mpaka Mwaka wa
Yubile. Mali hiyo itarudishwa mwaka wa
Yubile, naye ataweza kuirudia mali yake.
29 “ ‘Ikiwa mtu atauza nyumba iliyo
ndani ya mji uliozungukwa kwa ukuta,
yeye anayo haki ya kuikomboa mwaka
mzima baada ya mauzo ya hiyo nyumba.
Wakati huo anaweza kuikomboa. 30 Ikiwa
haikukombolewa kabla ya mwaka mmoja
kamili kupita, nyumba iliyo ndani ya mji
uliozungukwa kwa ukuta itakuwa mali
ya kudumu ya mnunuzi na wazao wake.
Haitarudishwa mwaka wa Yubile. 31 Lakini
nyumba zilizo vijijini bila ya kuwa na
kuta zilizozizunguka zitahesabiwa kama
mashamba. Zinaweza kukombolewa, nazo
zirudishwe katika mwaka wa Yubile.
32 [k]“ ‘Walawi siku zote wana haki ya
kukomboa nyumba zao katika miji ya
Walawi wanayoimiliki. 33 Kwa hiyo mali
ya Mlawi inaweza kukombolewa, yaani
nyumba iliyouzwa katika mji wowote
wanaoushikilia itarudishwa mwaka wa

[a]**25:14** Law 19:13; 1Sam 12:3-4; 1Kor 6:8; Za 10:18; Mik 2:2
[b]**25:15** Law 27:18, 23
[c]**25:17** Law 19:13, 14, 32; Ay 31:16; Mit 22:22; Yer 7:5-6; 21:12; 22:3; Zek 7:9-10; 1The 4:6; Mit 14:31; Eze 22:29
[d]**25:18** Mwa 26:5; Law 26:4-5; Kum 12:10; 33:28; Ay 5:22; Za 4:8; Yer 23:6; 30:10; 32:37; 33:16; Eze 28:26; 34:25; 38:14
[e]**25:19** Law 26:4; Kum 11:14; 28:12; Isa 55:10; Mt 6:25; Hes 11:4-13; 2Fal 6:15
[f]**25:21** Kum 28:8-12; Za 133:3; 134:3; 147:13; Eze 44:30; Hag 2:19; Mal 3:10; Kut 16:5
[g]**25:22** Law 26:10; 2Fal 19:29; Yos 5:11
[h]**25:23** Hes 36:7; 1Fal 21:3; Eze 46:18; Kut 19:5; Mwa 23:4; Ebr 11:13
[i]**25:24** Rut 4:7; Yer 32:8
[j]**25:25** Rut 2:20; 4:4; Yer 32:7; Law 27:13-31
[k]**25:32** Hes 35:1-8; Yos 21:2

Yubile, kwa sababu nyumba zilizo katika
miji ya Walawi ni mali yao miongoni mwa
Waisraeli. 34 [a]Lakini nchi ya malisho iliyo
mali ya miji yao kamwe isiuzwe, ni milki
yao ya kudumu.

35 [b]" 'Ikiwa mmoja wa wazawa wa nchi
yako amekuwa maskini, naye akashindwa
kujitegemeza mwenyewe katikati yako,
msaidie kama vile ambavyo ungelimsaidia
mgeni au kama mkazi wa muda, ili
aweze kuendelea kuishi katikati yako.
36 [c]Usichukue riba wala faida yoyote kutoka
kwake, bali utamwogopa Mungu wako, ili
mzawa wa nchi yako aweze kuendelea
kuishi katikati yako. 37 [d]Usimkopeshe fedha
ili alipe na riba, wala usimuuzie chakula
kwa faida. 38 [e]Mimi ndimi BWANA Mungu
wako, niliyekuleta kutoka nchi ya Misri
nikupe nchi ya Kanaani, nami niwe Mungu
wako.

39 [f]" 'Ikiwa mmoja wa wazawa wa nchi
yako amekuwa maskini katikati yako,
naye akajiuza kwako, usimfanye atumike
kama mtumwa. 40 Atatendewa kama
mfanyakazi aliyeajiriwa, au kama mkazi
wa muda katikati yako, naye atatumika
mpaka Mwaka wa Yubile. 41 Ndipo yeye
na watoto wake wataachiwa, naye atarudi
kwa watu wa ukoo wake, na kwenye mali
ya baba zake. 42 [g]Kwa sababu Waisraeli ni
watumishi wangu niliowaleta kutoka nchi
ya Misri, kamwe wasiuzwe kama watumwa.
43 [h]Usiwatawale kwa ukatili, lakini utamcha
Mungu wako.

44 " 'Watumwa wako wa kiume na wa kike
watatoka katika mataifa yanayokuzunguka;
kutoka kwao waweza kununua watumwa.
45 Pia waweza kununua baadhi ya wakazi
wa muda wanaoishi katikati yako, na jamaa
ya koo zao waliozaliwa katika nchi yako,
nao watakuwa mali yako. 46 Hao waweza
kuwarithisha watoto wako kuwa urithi wao,
na wanaweza kuwafanya watumwa maisha
yao yote, lakini usiwatawale ndugu zako
Waisraeli kwa ukatili.

47 [i]" 'Ikiwa mgeni au mkazi wa muda
katikati yako atakuwa tajiri, na mmoja wa
wazawa wa nchi yako akawa maskini, naye
akajiuza kwa yule mgeni anayeishi katikati
yako, au kwa mmoja wa jamaa wa koo za
wageni, 48 anayo haki ya kukombolewa
baada ya kujiuza. Mmoja wa jamaa zake
aweza kumkomboa: 49 Mjomba wake, au
binamu yake, au yeyote aliye ndugu wa
damu katika ukoo wake aweza kumkomboa.
Au ikiwa atafanikiwa, anaweza kujikomboa
mwenyewe. 50 [j]Yeye na huyo aliyemnunua
watahesabu muda kuanzia mwaka aliojiuza
hadi Mwaka wa Yubile. Mahali pa kuanzia
bei ya kuachiwa kwake itakadiriwa kwa
ujira unaolipwa mfanyakazi aliyeajiriwa
kwa idadi ya hiyo miaka. 51 Ikiwa imebaki
miaka mingi, ni lazima atalipia ukombozi
wake fungu kubwa la bei iliyolipwa
kumnunua yeye. 52 Ikiwa miaka iliyobaki
ni michache kufikia Mwaka wa Yubile,
atafanya hesabu yake, naye atalipa malipo
yanayostahili kwa ajili ya ukombozi wake.
53 [k]Atatendewa kama mtu wa kuajiriwa
mwaka hadi mwaka; lazima uone kwamba
yule aliyemnunua hamtawali kwa ukatili.

54 " 'Hata ikiwa hakukombolewa kwa njia
mojawapo ya hizi, yeye na watoto wake
wataachiwa katika Mwaka wa Yubile,
55 [l]kwa maana Waisraeli ni mali yangu
kama watumishi. Wao ni watumishi wangu,
niliowatoa kutoka nchi ya Misri. Mimi
ndimi BWANA Mungu wako.

---

[a]**25:34** Hes 35:2-5; Eze 48:14; Mdo 4:36
[b]**25:35** Kum 24:14-15; 15:8; Za 37:21-26; Mit 21:26; Lk 6:35; Mdo 11:29; Rum 12:18; 1Yn 3:17; Kum 15:7
[c]**25:36** Kut 22:25; Yer 15:10; Law 19:32; Kum 23:19; Neh 5:7; Za 15:5; Mit 28:8; Eze 18:8
[d]**25:37** Kut 22:25
[e]**25:38** Mwa 10:19; 17:7; Law 11:45
[f]**25:39** 1Fal 5:13; 9:23; Yer 34:14; Kut 21:2; 22:3; Kum 15:12
[g]**25:42** Rum 6:22; 1Kor 7:23
[h]**25:43** Kut 1:13; Eze 34:4; Kol 4:1; Mwa 42:18; Isa 47:6; Efe 6:9; Kum 25:18; Mal 3:5
[i]**25:47** Neh 5:5; Ay 24:9
[j]**25:50** Ay 7:1; 14:6; Isa 16:14; 21:16
[k]**25:53** Kol 4:1
[l]**25:55** Law 11:44-45

*Thawabu Ya Utii*

**(Kumbukumbu 7:12-24; 28:1-14)**

26 [a]“ ‘Msijitengenezee sanamu au kusimamisha kinyago cha kuchonga, au mnara, wala jiwe la kuabudia, na pia msijiwekee jiwe lililochongwa katika nchi yenu na kusujudu mbele yake. Mimi ndimi BWANA Mungu wenu.

2 [b]“ ‘Zishikeni Sabato zangu na kuheshimu mahali patakatifu pangu. Mimi ndimi BWANA.

3 [c]“ ‘Ikiwa mtafuata amri zangu na kuwa waangalifu kutii maagizo yangu,
4 [d]nitawanyeshea mvua katika majira yake, nayo ardhi itatoa mazao yake, na miti ya mashambani itazaa matunda yake.
5 [e]Kupura nafaka kwenu kutaendelea mpaka wakati wa kuvuna zabibu. Pia kuvuna zabibu kutaendelea mpaka wakati wa kupanda mbegu, nanyi mtakula na kushiba, na mtaishi salama katika nchi yenu.

6 [f]“ ‘Nitawapa amani katika nchi, mpate kulala pasipo kutiwa hofu na yeyote. Nitawaondoa wanyama wakali watoke kwenye nchi, nao upanga hautapita katika
nchi yenu. 7 [g]Mtawafukuza adui zenu, nanyi
mtawaua kwa upanga mbele yenu. 8 [h]Watu
wenu watano watafukuza adui mia, watu wenu mia watafukuza adui elfu kumi, nao adui zenu wataanguka kwa upanga mbele yenu.

9 [i]“ ‘Nitawaangalia kwa upendeleo na kuwafanya mzae na kuzidisha idadi yenu, nami nitalishika Agano langu na ninyi.
10 [j]Wakati wa kuvuna mtakuwa bado mnakula mavuno ya mwaka uliopita, na itawalazimu kuyaondoa ghalani ili mpate
nafasi ya mavuno mapya. 11 [k]Nitafanya
makao yangu miongoni mwenu, nami
sitawachukia. 12 [l]Nitatembea katikati yenu
niwe Mungu wenu, nanyi mtakuwa watu
wangu. 13 [m]Mimi ndimi BWANA Mungu
wenu, niliyewatoa katika nchi ya Misri ili msiendelee kuwa watumwa wa Wamisri, nikavunja kongwa lenu, na kuwawezesha kutembea mkiwa mmeinua vichwa vyenu juu.

*Adhabu Ya Kutokutii*

**(Kumbukumbu 28:15-68)**

14 [n]“ ‘Lakini kama hamtanisikiliza na
kutimiza maagizo haya yote, 15 [o]nanyi kama
mtazikataa amri zangu na kuzichukia sheria zangu, tena mkishindwa kutimiza amri zangu na hivyo mkavunja agano langu,
16 [p]ndipo nitakapowafanyia hili: Nitawaletea juu yenu hofu ya ghafula, magonjwa ya kufisha, na homa itakayopofusha macho yenu na kuwaondolea uhai wenu. Mtapanda mbegu bila mafanikio, kwa sababu adui
zenu wataila. 17 [q]Nitauelekeza uso wangu
dhidi yenu ili mshindwe na adui zenu;

---

[a]**26:1** Kut 20:4; 23:24; Za 97:2; Isa 48:5; Yer 44:9; Hab 2:18; Hes 33:52; Kum 4:16-19; Isa 44:9-20; Za 97:7
[b]**26:2** Kut 20:8; Law 19:30
[c]**26:3** Mwa 26:5; Kut 24:8; Kum 6:17; 7:12; 11:13, 22; 28:1, 9
[d]**26:4** Kum 11:14; 28:12; Za 65:9; 67:6; 68:9; 104:13; 147:8; Yer 5:24; Hos 6:3; Yoe 2:23; Zek 10:1; Ay 5:10; 14:9; Kut 23:24; Law 25:19
[e]**26:5** Kum 6:11; 11:15; Eze 36:29-30; Yoe 2:19, 26; Law 25:18
[f]**26:6** Za 3:5; 4:8; 29:11; 37:11; 85:8; 147:14; Isa 17:2; 26:3; 54:13; 60:18; Hag 2:9; Mit 3:24; Ay 11:18-19; Yer 30:10; Mik 4:4; Sef 3:13; Mwa 37:20
[g]**26:7** Za 18:37; 44:5
[h]**26:8** Isa 30:17; Kum 28:7; 32:30; Yos 23:10; Amu 15:15; 1Nya 12:14
[i]**26:9** Mwa 1:22; 17:6, 7; Neh 9:23; Kut 2:25; 2Fal 13:23
[j]**26:10** Law 25:22
[k]**26:11** Kut 25:8; Za 74:7; 76:2; Eze 37:27; Kum 31:6; 1Sam 12:22; 1Fal 6:13; 2Fal 17:15
[l]**26:12** Mwa 3:8; 17:7; Kut 6:7; Yer 7:23; 11:4; 24:7; 30:22; 31:1; Zek 13:9; 2Kor 6:16; Efe 2:21; Ebr 3:6; Eze 11:20
[m]**26:13** Law 11:44; Kut 6:6; 13:3; Isa 10:27; Yer 2:20; 27:2; 28:10; 30:8; Eze 30:18; 34:27; Hos 11:4
[n]**26:14** Kum 28:15-68; Mal 2:2
[o]**26:15** Mwa 17:7; 2Fal 17:15
[p]**26:16** Kum 28:22, 35; Za 78:33; 107:17; 1Sam 2:33; Eze 4:17; 24:23; 33:10; Amu 6:3-6; Ay 31:8
[q]**26:17** Law 17:10; Eze 15:7; Kum 28:7, 25, 48; Yos 7:4, 12; Amu 2:15; 1Fal 8:33; 2Nya 6:24; Yer 9:17; 21:7; Za 106:41; 53:5; Mit 28:1; Isa 30:17

wale wanaowachukia watawatawala,
nanyi mtakimbia ingawa hakuna mtu
anayewafukuza.
18 [a]“ ‘Kama baada ya haya yote
hamtanisikiliza, nitawaadhibu mara
saba zaidi kwa ajili ya dhambi zenu.
19 [b]Nitakivunja kiburi chenu cha ukaidi
na kuifanya anga iliyo juu yenu iwe kama
chuma, na ardhi yenu kama shaba. 20 [c]Nguvu
zenu zitatumika bila ya mafanikio, kwa
sababu ardhi yenu haitawazalia mazao
yake, wala miti ya nchi yenu haitazaa
matunda yake.
21 [d]“ ‘Kama mtaendelea kuwa na
uadui nami, na kukataa kunisikiliza,
nitawazidishia mateso yenu mara saba
zaidi, kama dhambi zenu zinavyostahili.
22 [e]Nitawatuma wanyama mwitu dhidi
yenu, nao watawaibieni watoto wenu,
watawaangamiza ng’ombe wenu, na
kuifanya idadi yenu kuwa ndogo, hivi
kwamba barabara zenu zitakuwa hazina
watu.
23 [f]“ ‘Ikiwa pamoja na mambo haya
hamtakubali maonyo yangu lakini
mkaendelea kuweka uadui nami, 24 [g]mimi
mwenyewe nitaweka uadui nanyi, na
kuwatesa kwa ajili ya dhambi zenu mara
saba zaidi. 25 [h]Nitawaletea upanga juu yenu
ili kuwapatiliza kwa kuvunja Agano langu.
Mtakapokimbilia mijini mwenu, nitatuma
tauni katikati yenu, nanyi mtatiwa mikononi
mwa adui zenu. 26 [i]Nitakapowaondolea
upatikanaji wa mkate wenu, wanawake
kumi wataoka mkate wenu katika tanuru
moja, nao wataugawa mkate kidogo kwa
kupima. Mtakula, lakini hamtashiba.
27 “ ‘Kama hata baada ya haya bado
hamtanisikiliza lakini mkaendelea kuweka
uadui nami, 28 [j]ndipo katika hasira yangu
nitaweka uadui nanyi, nami mwenyewe
nitawaadhibu mara saba kwa ajili ya dhambi
zenu. 29 [k]Mtakula nyama ya wana wenu
na nyama ya binti zenu. 30 [l]Nitapaharibu
mahali penu pa juu pa kuabudia miungu,
nibomoe madhabahu zenu za kufukizia
uvumba, na kuzilundika maiti zenu juu
ya sanamu zenu zisizo na uhai, nami
nitawachukia ninyi sana. 31 [m]Nitaifanya
miji yenu kuwa magofu, na kuharibu
mahali patakatifu penu pa kuabudia, nami
sitapendezwa na harufu nzuri ya sadaka
zenu. 32 [n]Nitaiharibu nchi, ili adui zenu
watakaokuja kuishi humo washangae.
33 [o]Nitawatawanya ninyi miongoni mwa
mataifa, na kuufuta upanga wangu na
kuwafuatia. Nchi yenu itaharibiwa, nayo
miji yenu itakuwa magofu. 34 [p]Ndipo nchi
itafurahia Sabato zake muda wote ule

[a]**26:18** Za 99:8; Yer 21:14; Amo 3:14
[b]**26:19** Za 10:4; 73:6; Isa 16:6; 25:11; 28:1-3; Yer 13:9; 48:29; Eze 24:21; Amo 6:8; Sef 3:11; Kum 28:23; Ay 28:28
[c]**26:20** Kum 11:17; 28:24, 38; Za 127:1; Isa 17:11; 49:4; Yer 12:13; Mik 6:15; Hag 1:6
[d]**26:21** Mwa 4:15
[e]**26:22** Mwa 37:20; Kum 28:62; Yer 42:2; 5:6; 14:16; 15:3; 16:4; Eze 14:15
[f]**26:23** Yer 2:30; 5:3; 7:28; 17:23; 32:33; Sef 3:2
[g]**26:24** 2Sam 22:27
[h]**26:25** Yer 5:17; 15:3; 47:6; 50:28; 51:6, 11; Eze 11:8; 14:17; 21:4; 33:2; Kut 5:3; 9:3; Hes 16:46; 1Fal 8:37; Hab 3:5
[i]**26:26** 1Fal 8:37; 18:2; 2Fal 4:38; 6:25; 25:3; Za 105:16; Isa 3:1; 9:20; Yer 37:21; 52:6; Eze 4:16-17; 5:16; 14:13; Hos 4:10; Mik 6:14
[j]**26:28** Kum 32:19; Amu 2:14; Za 78:59; 106:40; Kum 7:10; Ay 34:11; Isa 59:18; 65:5-7; 66:6; Yer 17:10; 25:29; Yoe 3:4
[k]**26:29** 2Fal 6:29; Yer 19:6; Mao 4:10; Eze 5:10; Kum 28:53
[l]**26:30** Kum 12:2; 1Sam 9:12; 10:5; 1Fal 3:2, 4; 12:31; 13:2, 32; 2Fal 17:29; 23:20; 2Nya 34:3, 4; Za 78:58; 106:40; Eze 6:3, 6, 13; 16:16; Amo 6:8; 7:9; Isa 17:8; 27:9; 21:9; Yer 50:2
[m]**26:31** Neh 1:3; Isa 1:7; 3:8, 26; 6:11; 24:12; 61:4; 63:18; 64:11; Yer 4:7; 9:11; 25:11; 34:22; 44:2-6, 22; Eze 36:33; 24:21; Mik 2:4; 3:12; Sef 2:5; 3:6; 2Fal 22:19; Za 74:3-7; Mao 2:7; Amo 7:9; 5:21; 8:10
[n]**26:32** Isa 5:6; 52:14; Yer 9:11; 12:11; 25:11; 26:9; 33:10; 34:22; 44:22; 18:16; 19:8; 48:39; 1Fal 9:8; 2Nya 29:8; Eze 5:14; 26:16; 27:35; 28:19
[o]**26:33** Yer 4:11; 7:34; 9:16; 13:24; 31:10; 40:3, 15; 50:17; 42:16; Eze 5:10; 12:15; 17:21; 20:23; 22:15; 34:6; Yoe 3:2; Kum 4:27; 28:64; Neh 1:8; Za 44:11; 106:27; Zek 7:14; Amo 9:4; Isa 49:19; 1Sam 15:22; Ay 36:11
[p]**26:34** Isa 1:7; Yer 7:34; 25:11; 44:6; Eze 33:29; 2Nya 36:21

itakapokuwa ukiwa, nanyi mkiwa katika
nchi ya adui zenu. Ndipo nchi itapumzika
na kufurahia Sabato zake. 35 [a]Wakati wote
nchi itakapobaki ukiwa, itapumzika na
kufurahia Sabato zake ambazo haikuzipata
mlipokuwa mnaishi humo.

36 [b]“ ‘Kwa habari ya wenzenu wale
watakaobaki, nitaifanya mioyo yao kuwa
na hofu kuu katika nchi za adui zao, kiasi
kwamba sauti ya jani linalopeperushwa
na upepo itawafanya wakimbie.
Watakimbia kana kwamba wanakimbia
upanga, nao wataanguka, ingawa hakuna
anayewafukuza. 37 [c]Watajikwaa mmoja juu
ya mwingine kama wakimbiao upanga,
hata ingawa hakuna anayewafuatia. Hivyo
hamtaweza kusimama mbele ya adui
zenu. 38 [d]Mtaangamia katikati ya mataifa;
nchi ya adui zenu itawala. 39 [e]Wale wenu
watakaobaki wataangamia katika nchi
za adui zao kwa sababu ya dhambi zao;
pia kwa sababu ya dhambi za baba zao
wataangamia.

40 [f]“ ‘Lakini kama watatubu dhambi
zao na dhambi za baba zao, udanganyifu
wao dhidi yangu na uadui wao kwangu,
41 [g]ambao ulinifanya niwe na uadui nao
hata nikawapeleka katika nchi ya adui
zao, wakati mioyo yao isiyotahiriwa
itanyenyekea na kutubu dhambi yao,
42 [h]nami nitakumbuka agano langu na
Yakobo, na agano langu na Isaki, na agano
langu na Abrahamu, nami nitaikumbuka
nchi. 43 Kwa kuwa wataiacha nchi ukiwa,
nayo itafurahia Sabato zake wakati itakuwa
ukiwa bila wao. Wataadhibiwa kwa ajili
ya dhambi zao, kwa sababu walizikataa
sheria zangu na kuzichukia amri zangu.
44 [i]Lakini pamoja na hili, wakati watakuwa
katika nchi ya adui zao, sitawakataa wala
kuwachukia kiasi cha kuwaharibu kabisa
na kuvunja agano langu nao. Mimi ndimi
BWANA Mungu wao. 45 [j]Lakini kwa ajili yao
nitalikumbuka agano langu na baba zao,
ambao niliwatoa Misri mbele ya mataifa ili
niwe Mungu wao. Mimi ndimi BWANA.’ ”

46 [k]Hizi ndizo amri, sheria na pia
masharti ambazo BWANA alifanya kati yake
mwenyewe na Waisraeli katika Mlima Sinai
kupitia kwa Mose.

### *Kukomboa Kile Kilicho Cha BWANA*

27 BWANA akamwambia Mose, 2 [l]“Sema
na Waisraeli uwaambie: ‘Kama mtu
yeyote ataweka nadhiri maalum ili kuweka
watu wakfu kwa BWANA, kwa kutoa kiasi
cha thamani inayolingana, 3 [m]thamani
ya kukomboa mwanaume mwenye kati
ya umri wa miaka ishirini na miaka
sitini itakuwa shekeli hamsini[n] za fedha,
kulingana na shekeli ya mahali patakatifu;
4 ikiwa ni mwanamke, weka thamani yake
kwa shekeli thelathini.[o] 5 [p]Kama ni mtu
mwenye umri wa miaka kati ya mitano na
ishirini, weka thamani ya mwanaume kuwa
shekeli ishirini,[q] na mwanamke shekeli
kumi.[r] 6 [s]Kama ni mtu mwenye umri kati
ya mwezi mmoja na miaka mitano, weka
thamani ya mwanaume kuwa shekeli tano
za fedha, na ile ya mwanamke kuwa shekeli

---

[a]**26:35** Law 25:4
[b]**26:36** Ay 13:25; 2Fal 25:5; Za 58:7; Mao 1:3-6; 4:19; Eze 21:7
[c]**26:37** Yer 6:21; 13:16; 46:16; Eze 3:20; Nah 3:3; Yos 7:12
[d]**26:38** Ay 4:9; 36:12; Isa 1:28; Yer 16:4; 44:27; Kum 4:26
[e]**26:39** Kut 20:5; Isa 14:21; 24:16; Eze 4:17
[f]**26:40** Law 5:5; Za 32:5; 38:18; 106:6; Neh 9:2; Yer 3:12-15; 14:20; Hos 5:15; Lk 15:18; 1Yn 1:9
[g]**26:41** Kum 10:16; 4:31; 30:6; Yer 4:4; 9:25-26; 4:27; 5:10; 30:11; 31:37; 33:26; 51:5; Eze 20:43; 44:7-9; Mdo 7:51; 2Nya 7:14; 12:6; Isa 6:7; 33:24; 40:2; 53:6-11; Amu 2:1
[h]**26:42** Za 69:25; 106:24; Isa 6:11; 32:14; 62:4; Yer 2:15; 44:2; Eze 20:13; 36:4; Hes 11:20; 14:31; 1Sam 8:7
[i]**26:44** 2Fal 17:20; 25:11; 2Nya 6:36; 36:20; Rum 11:2; Kut 6:8; Law 25:38
[j]**26:45** Kum 4:31
[k]**26:46** Kut 19:11; Law 7:38; 27:34
[l]**27:2** Mwa 28:20; Hes 6:2; Kum 23:21-23; Amu 11:30-39; Ay 22:27; Yn 1:16; Mdo 21:23
[m]**27:3** Kut 30:13; Hes 3:47; 18:16; Eze 45:12
[n]3 Shekeli 50 za fedha ni sawa na gramu 600.
[o]4 Shekeli 30 za fedha ni sawa na gramu 360.
[p]**27:5** Mwa 37:28
[q]5 Shekeli 20 za fedha ni sawa na gramu 240.
[r]5 Shekeli 10 za fedha ni sawa na gramu 120.
[s]**27:6** Hes 3:47; 18:16

tatu[a] za fedha. 7 Kama ni mtu mwenye
miaka sitini na zaidi, weka thamani ya
mwanaume kuwa shekeli kumi na tano,[b]
na mwanamke shekeli kumi. 8 [c]Kama mtu
yeyote anayeweka nadhiri ni maskini
mno kuweza kulipa kiasi kilichowekwa,
atampeleka huyo mtu kwa kuhani, ambaye
ataweka thamani yake kulingana na kile
mweka nadhiri anachoweza kulipa.

9 [d]“ ‘Kama kile mtu alichokiwekea
nadhiri ni mnyama anayekubalika kama
sadaka kwa Bwana, mnyama wa namna
hiyo aliyetolewa kwa Bwana anakuwa
mtakatifu. 10 Mtu haruhusiwi kumbadilisha
au kutoa mnyama mzuri kwa mbaya, au
mnyama mbaya kwa mzuri. Kama atatoa
mnyama badala ya mwingine, wanyama
wote wawili, yaani yule aliyetolewa na
yule aliyebadiliwa, ni watakatifu. 11 [e]Kama
alichokiwekea nadhiri ni mnyama aliye
najisi kiibada, yaani yule asiye kubalika
kuwa sadaka kwa Bwana, huyo mnyama
lazima aletwe kwa kuhani, 12 ambaye
ataamua ubora wa mnyama huyo, kama
ni mzuri au mbaya. Thamani yoyote
atakayoweka kuhani, hivyo ndivyo
itakavyokuwa. 13 [f]Kama mwenye mnyama
atapenda kumkomboa mnyama huyo,
lazima aongeze sehemu ya tano ya thamani
yake.

14 [g]“ ‘Kama mtu ataweka nyumba yake
wakfu kama kitu kitakatifu kwa Bwana,
kuhani ataamua ubora wa nyumba hiyo,
kama ni nzuri au mbaya. Thamani yoyote
kuhani atakayoweka, basi hivyo ndivyo
itakavyokuwa. 15 Kama mtu aliyeweka
nyumba yake wakfu ataikomboa, lazima
aongeze sehemu ya tano ya thamani yake,
nayo nyumba itakuwa yake tena.

16 “ ‘Kama mtu anaweka sehemu ya ardhi
ya jamaa yake wakfu kwa Bwana, thamani
yake itawekwa kulingana na kiasi cha mbegu
inayohitajiwa kupandwa katika ardhi hiyo,
yaani homeri[h] moja ya mbegu za shayiri
kwa shekeli hamsini za fedha. 17 Kama
akiweka shamba lake wakfu katika Mwaka
wa Yubile, ile thamani iliyokwisha wekwa
itakuwa iyo hiyo. 18 [i]Lakini kama akiweka
shamba lake wakfu baada ya Yubile, kuhani
ataweka thamani kulingana na idadi ya
miaka iliyobaki kufikia Mwaka wa Yubile
unaofuata, na thamani yake iliyoamuliwa
itapunguzwa. 19 [j]Kama mtu anayeweka
wakfu shamba anataka kulikomboa, lazima
aongeze sehemu ya tano ya thamani yake,
nalo shamba litakuwa lake tena. 20 Kama
pengine halikomboi shamba hilo, au kama
ameliuza kwa mtu mwingine, kamwe
haliwezi kukombolewa. 21 [k]Shamba hilo
litakapoachiwa mwaka wa Yubile, litakuwa
takatifu, kama shamba lililotolewa kwa
Bwana, nalo litakuwa mali ya makuhani.

22 “ ‘Kama mtu ameweka wakfu kwa
Bwana shamba alilonunua, ambalo si
sehemu ya ardhi ya jamaa yake, 23 [l]kuhani
ataamua thamani yake hadi Mwaka wa
Yubile, naye huyo mtu atalazimika kulipa
thamani yake siku hiyo kama kitu kitakatifu
kwa Bwana. 24 [m]Katika Mwaka wa Yubile,
shamba litarudishwa kwa mtu yule ambaye
lilinunuliwa kutoka kwake, yule ambaye
ardhi ilikuwa mali yake. 25 [n]Kila thamani
lazima iwekwe kulingana na shekeli ya
mahali patakatifu,[o] gera ishirini kwa shekeli.

26 [p]“ ‘Lakini hakuna mtu atakayeweka
wakfu mzaliwa wa kwanza wa mnyama,
kwa kuwa mzaliwa wa kwanza tayari ni
mali ya Bwana; awe ng’ombe au kondoo,
ni wa Bwana. 27 Kama ni mmoja wa

[a]6 Shekeli tatu za fedha ni sawa na gramu 36.
[b]7 Shekeli 15 za fedha ni sawa na gramu 180.
[c]**27:8** Law 5:11; 12:8; 14:21-22; Lk 21:1; 2Kor 8:12
[d]**27:9** Mwa 28:20; Kut 40:9; Hes 6:20; 18:17; Kum 15:19
[e]**27:11** Kut 13:13; Hes 18:15
[f]**27:13** Law 25:25; 5:16
[g]**27:14** Law 25:29-31; Hes 18:14; 2Kor 9:10
[h]16 Homeri moja ni sawa na efa 10, ambazo ni sawa na kilo 100.
[i]**27:18** Law 25:10-15; 25:15-16
[j]**27:19** Law 25:25
[k]**27:21** Law 25:10; Hes 18:14; Eze 44:29
[l]**27:23** Law 25:15
[m]**27:24** Law 25:28
[n]**27:25** Kut 30:13; Hes 3:47; Eze 45:12; Hes 18:16
[o]25 Shekeli moja ya mahali patakatifu ni sawa na gramu 11.
[p]**27:26** Kut 13:12; 22:30; Hes 18:17; Kut 15:19

wanyama walio najisi, aweza kumnunua
kwa bei iliyowekwa, akiongeza sehemu ya
tano ya thamani yake. Kama hatamkomboa,
mnyama huyo atauzwa kwa bei iliyowekwa.
28 [a]“ ‘Lakini chochote kile mtu alicho
nacho na akakiweka wakfu[b] kwa BWANA,
iwe ni binadamu, au mnyama, au ardhi ya
jamaa, hakiwezi kuuzwa au kukombolewa.
Chochote kilichowekwa wakfu ni kitakatifu
sana kwa BWANA.
29 [c]“ ‘Mtu yeyote aliyewekwa wakfu ili
kuangamizwa, hawezi kukombolewa. Mtu
kama huyo lazima auawe.
30 [d]“ ‘Zaka ya kila kitu kutoka shambani,
iwe ni nafaka kutoka kwa ardhi, au tunda
kutoka kwa miti, ni mali ya BWANA;
ni takatifu kwa BWANA. 31 [e]Kama mtu
akikomboa chochote cha zaka yake, lazima
aongeze sehemu ya tano ya thamani yake.
32 [f]Zaka yote ya kundi la ng’ombe au la
kondoo na mbuzi, kila mnyama wa kumi
apitaye chini ya fimbo ya yule awachungaye,
atakuwa mtakatifu kwa BWANA. 33 [g]Yule
mnyama wa kumi hatachaguliwa kwa
kigezo cha uzuri au ubaya, naye haruhusiwi
kubadiliwa. Ikiwa atabadiliwa, basi mnyama
yule wa kwanza na huyo aliyebadiliwa
wote watahesabiwa kuwa watakatifu, na
haiwezekani kuwakomboa.’ ”
34 [h]Haya ndiyo maagizo BWANA aliyompa
Mose juu ya Mlima Sinai kwa ajili ya
Waisraeli.

---

[a]**27:28** Hes 18:14; Yos 6:17-19; Amu 11:30-31
[b]28 *Akakiweka wakfu* ina maana ya kumpa Mungu kabisa, daima, bila kurudiwa.
[c]**27:29** Kum 7:26
[d]**27:30** Hes 18:26; Kum 7:6; 12:6, 17; 14:22-28; 2Nya 31:6; Neh 10:37; 12:44; 13:5; Mal 3:8; Ezr 9:2; Isa 6:13
[e]**27:31** Law 25:25; 5:16
[f]**27:32** Za 89:32; Yer 33:13; Eze 20:37; Mik 7:14
[g]**27:33** Hes 18:21
[h]**27:34** Kut 19:11; Law 7:38; Kum 4:5; Mdo 7:38

# HESABU

*Watu Wahesabiwa Kwa Mara Ya Kwanza*

1 [a]BWANA alisema na Mose katika Jangwa
la Sinai, katika Hema la Kukutania, siku
ya kwanza ya mwezi wa pili, katika mwaka
wa pili baada ya Waisraeli kutoka nchi ya
Misri. Akamwambia, 2 [b]"Hesabu watu wa
jumuiya yote ya Waisraeli kwa kufuata
koo zao na jamaa zao, ukiorodhesha
kila mwanaume kwa jina lake, mmoja
mmoja. 3 [c]Wewe na Aroni mtawahesabu
kwa migawanyo yao wanaume wote
katika Israeli wenye miaka ishirini na
kuendelea ambao wanaweza kutumika
katika jeshi. 4 [d]Mwanaume mmoja kutoka
kila kabila, kila aliye kiongozi wa jamaa
yake, atawasaidia. 5 [e]Haya ndiyo majina ya
wanaume watakaowasaidia:

"kutoka Reubeni, ni Elisuri mwana wa Shedeuri;
6 [f]kutoka Simeoni, ni Shelumieli mwana wa Surishadai;
7 [g]kutoka Yuda, ni Nashoni mwana wa Aminadabu;
8 [h]kutoka Isakari, ni Nethaneli mwana wa Suari;
9 [i]kutoka Zabuloni, ni Eliabu mwana wa Heloni;
10 [j]kutoka wana wa Yosefu:
kutoka Efraimu, ni Elishama mwana wa Amihudi;
kutoka Manase, ni Gamalieli mwana wa Pedasuri;
11 [k]kutoka Benyamini, ni Abidani mwana wa Gideoni;
12 [l]kutoka Dani, ni Ahiezeri mwana wa Amishadai;
13 [m]kutoka Asheri, ni Pagieli mwana wa Okrani;
14 [n]kutoka Gadi, ni Eliasafu mwana wa Deueli;
15 [o]kutoka Naftali, ni Ahira mwana wa Enani."

16 [p]Hawa walikuwa wanaume
walioteuliwa kutoka jumuiya, viongozi wa
makabila ya baba zao. Walikuwa wakuu
wa koo za Israeli.
17 Mose na Aroni wakawachukua
wanaume hao waliokuwa wamepewa
majina yao, 18 [q]wakaita jumuiya yote pamoja
katika siku ya kwanza ya mwezi wa pili.
Watu wakaonyesha nasaba zao kwa koo zao
na jamaa zao, nao wanaume waliokuwa na
miaka ishirini au zaidi waliorodheshwa kwa
majina, mmoja mmoja, 19 [r]kama BWANA
alivyomwagiza Mose. Hivyo aliwahesabu
katika Jangwa la Sinai:

20 [s]Kutoka wazao wa Reubeni, mzaliwa wa kwanza wa kiume wa Israeli:
Wanaume wote waliokuwa na miaka ishirini au zaidi ambao waliweza kutumika katika jeshi waliorodheshwa kwa majina, mmoja mmoja, kufuatana na kumbukumbu za koo zao na jamaa

---

[a]**1:1** Kut 27:21; 40:2; 19:1; 6:14; 40:17; Hes 10:12
[b]**1:2** Kut 30:11-16; Hes 3:40; 26:2; 1Nya 21:2; 2Sam 24:2
[c]**1:3** Kut 4:14; 30:14; Hes 17:3; 26:2; Yos 5:4; 1Nya 5:18
[d]**1:4** Law 24:11; Hes 7:2; 30:1; 31:26; 34:18; Kut 18:21; Kum 1:15; Yos 22:14
[e]**1:5** Hes 2:10; 7:30; 10:18; 17:2; Mwa 29:32; Ufu 7:4-5
[f]**1:6** Hes 25:14; 2:12; 7:36; 10:19
[g]**1:7** Mwa 29:35; Za 78:68; Kut 6:23; Hes 7:12; Rut 4:20; 1Nya 2:10; Lk 3:32
[h]**1:8** Mwa 30:18; Hes 10:15; 2:5; 7:18
[i]**1:9** Hes 10:16; 2:7; 7:24
[j]**1:10** Hes 2:18, 20; 7:48-53; 10:22-23
[k]**1:11** Hes 10:24; 2:22; 7:60; Za 68:27
[l]**1:12** Hes 2:25; 7:66; 10:25
[m]**1:13** Hes 10:26; 2:27; 7:72
[n]**1:14** Hes 10:20; 2:14; 7:42
[o]**1:15** Hes 10:27; 2:29; 7:78
[p]**1:16** Kut 18:25; Hes 32:28; Mwa 6:4; 1Nya 5:24; Amu 6:15
[q]**1:18** Ezr 2:59; Ebr 7:3; Kut 30:14
[r]**1:19** Kut 30:12; Hes 26:63; 31:49
[s]**1:20** Mwa 10:15; 29:32; 46:9; Ufu 7:5

zao. 21 [a]Idadi kutoka kabila la
Reubeni ilikuwa watu 46,500.

22 [b]Kutoka wazao wa Simeoni:
Wanaume wote waliokuwa na miaka ishirini au zaidi ambao waliweza kutumika katika jeshi walihesabiwa na kuorodheshwa kwa majina, mmoja mmoja, kufuatana na kumbukumbu za koo
zao na jamaa zao. 23 [c]Idadi kutoka
kabila la Simeoni walikuwa watu 59,300.

24 [d]Kutoka wazao wa Gadi:
Wanaume wote waliokuwa na miaka ishirini au zaidi ambao waliweza kutumika katika jeshi waliorodheshwa kwa majina, kufuatana na kumbukumbu za koo
zao na jamaa zao. 25 [e]Idadi kutoka
kabila la Gadi walikuwa watu 45,650.

26 [f]Kutoka wazao wa Yuda:
Wanaume wote waliokuwa na miaka ishirini au zaidi ambao waliweza kutumika katika jeshi waliorodheshwa kwa majina, kufuatana na kumbukumbu za koo
zao na jamaa zao. 27 [g]Idadi kutoka
kabila la Yuda walikuwa watu 74,600.

28 [h]Kutoka wazao wa Isakari:
Wanaume wote waliokuwa na miaka ishirini au zaidi ambao waliweza kutumika katika jeshi waliorodheshwa kwa majina, kufuatana na kumbukumbu za koo
zao na jamaa zao. 29 [i]Idadi kutoka
kabila la Isakari walikuwa watu 54,400.

30 [j]Kutoka wazao wa Zabuloni:
Wanaume wote waliokuwa na miaka ishirini au zaidi ambao waliweza kutumika katika jeshi waliorodheshwa kwa majina, kufuatana na kumbukumbu za koo
zao na jamaa zao. 31 [k]Idadi kutoka
kabila la Zabuloni walikuwa watu 57,400.

32 [l]Kutoka wana wa Yosefu:
Kutoka wazao wa Efraimu:
Wanaume wote waliokuwa na miaka ishirini au zaidi ambao waliweza kutumika katika jeshi waliorodheshwa kwa majina, kufuatana na kumbukumbu za koo
zao na jamaa zao. 33 [m]Idadi kutoka
kabila la Efraimu walikuwa watu 40,500.

34 [n]Kutoka wazao wa Manase:
Wanaume wote waliokuwa na miaka ishirini au zaidi ambao waliweza kutumika katika jeshi waliorodheshwa kwa majina, kufuatana na kumbukumbu za koo
zao na jamaa zao. 35 Idadi kutoka
kabila la Manase walikuwa watu 32,200.

36 [o]Kutoka wazao wa Benyamini:
Wanaume wote waliokuwa na miaka ishirini au zaidi ambao waliweza kutumika katika jeshi waliorodheshwa kwa majina, kufuatana na kumbukumbu za koo
zao na jamaa zao. 37 [p]Idadi kutoka
kabila la Benyamini walikuwa watu 35,400.

---

[a]**1:21** Hes 26:7
[b]**1:22** Mwa 29:33; Ufu 7:7; 2Sam 22:35; Za 60:12; Efe 6:12
[c]**1:23** Hes 26:14
[d]**1:24** Mwa 30:11; Yos 13:24-28; Ufu 7:5
[e]**1:25** Mwa 46:16; Hes 26:18; 1Nya 5:11
[f]**1:26** Mt 1:2; Mwa 29:35; Ufu 7:5; Mwa 49:8-10; Za 78:68; Ebr 7:14
[g]**1:27** Hes 26:22
[h]**1:28** Mwa 30:18; Ufu 7:7
[i]**1:29** Mwa 30:18; Hes 26:25
[j]**1:30** Mwa 30:20; Ufu 7:8
[k]**1:31** Hes 26:27
[l]**1:32** Mwa 49:26; 41:52; Hes 26:35-37; Za 60:7; Yer 7:15
[m]**1:33** Hes 26:37; 1Nya 7:20
[n]**1:34** Mwa 41:51; Ufu 7:6
[o]**1:36** Mwa 35:18; 2Nya 17:17; Yer 32:44; Oba 1:19; Ufu 7:8
[p]**1:37** Hes 26:41

38 [a]Kutoka wazao wa Dani:
Wanaume wote waliokuwa na miaka ishirini au zaidi ambao waliweza kutumika katika jeshi waliorodheshwa kwa majina, kufuatana na kumbukumbu za koo zao na jamaa zao. 39 [b]Idadi kutoka kabila la Dani walikuwa watu 62,700.

40 [c]Kutoka wazao wa Asheri:
Wanaume wote waliokuwa na miaka ishirini au zaidi ambao waliweza kutumika katika jeshi waliorodheshwa kwa majina, kufuatana na kumbukumbu za koo zao na jamaa zao. 41 [d]Idadi kutoka kabila la Asheri walikuwa watu 41,500.

42 [e]Kutoka wazao wa Naftali:
Wanaume wote waliokuwa na miaka ishirini au zaidi ambao waliweza kutumika katika jeshi waliorodheshwa kwa majina, kufuatana na kumbukumbu za koo zao na jamaa zao. 43 [f]Idadi kutoka kabila la Naftali walikuwa watu 53,400.

44 [g]Hawa walikuwa wanaume waliohesabiwa na Mose, Aroni na viongozi kumi na wawili wa Israeli, kila mmoja akiwakilisha jamaa yake. 45 [h]Wanaume wote Waisraeli waliokuwa na miaka ishirini au zaidi ambao waliweza kutumika katika jeshi la Israeli walihesabiwa kufuatana na jamaa zao. 46 [i]Jumla ya hesabu yao ilikuwa watu 603,550.

47 [j]Hata hivyo, jamaa ya kabila la Lawi hawakuhesabiwa pamoja na wengine.
48 BWANA alikuwa amemwambia Mose:
49 [k]"Kamwe usihesabu kabila la Lawi wala kuwaweka pamoja katika hesabu ya Waisraeli wengine.
50 [l]Badala yake, waweke Walawi kuwa viongozi wa Maskani ya Ushuhuda, juu ya samani zake na kila kitu kilichomo ndani yake. Wao watabeba Maskani na samani zake zote; wataitunza na kupiga kambi kuizunguka.
51 [m]Wakati wowote Maskani inapohamishwa, Walawi wataifungua, na wakati wowote maskani inapotakiwa kusimamishwa, Walawi watafanya kazi hiyo. Mtu yeyote mwingine ambaye atasogea karibu nayo atauawa.
52 [n]Waisraeli watapiga mahema yao kwa makundi makundi, kila mwanaume katika kambi yake mwenyewe chini ya bendera yake.
53 [o]Hata hivyo, Walawi watapiga mahema yao kuzunguka Maskani ya Ushuhuda ili ghadhabu isiipate jumuiya ya Waisraeli. Walawi watawajibika kwa utunzaji wa Maskani ya Ushuhuda."

54 Waisraeli walifanya yote haya sawasawa kama BWANA alivyomwamuru Mose.

*Mpangilio Wa Kambi Za Makabila*

2 BWANA aliwaambia Mose na Aroni:
2 [p]"Waisraeli watapiga kambi zao kuzunguka Hema la Kukutania kwa umbali fulani kutoka kwenye hema, kila mwanaume chini ya alama yake pamoja na bendera ya jamaa yake."

3 [q]Kwa upande wa mashariki kuelekea mawio ya jua, kambi ya makundi ya Yuda watapiga kambi chini ya alama yao. Kiongozi wa watu wa Yuda ni Nashoni mwana wa

[a]**1:38** Mwa 30:6; Kum 33:22
[b]**1:39** Hes 26:43
[c]**1:40** Mwa 30:13; Hes 26:44; Ufu 7:6
[d]**1:41** Hes 26:47
[e]**1:42** Mwa 30:8; Ufu 7:6
[f]**1:43** Hes 26:50; Kut 1:1-4
[g]**1:44** Hes 26:64
[h]**1:45** Hes 14:29; 2:32
[i]**1:46** Kut 12:37; 2Sam 24:9; Mwa 13:16; Kut 38:26; Hes 26:51; 1Fal 4:20
[j]**1:47** Hes 3:17-20; 26:57; 4:3, 49; 1Nya 21:6
[k]**1:49** Hes 26:62
[l]**1:50** Kut 31:18; 15:9; 16:34; Mdo 7:44; Hes 4:15-33
[m]**1:51** Kut 21:12; 26:1; Hes 4:5, 15; 3:38
[n]**1:52** Hes 10:14; Za 20:4-5; Wim 2:4; 6:4
[o]**1:53** Hes 2:10; 3:23-38; 16:46; 18:2-5; Law 10:6; Kum 9:22; Kut 38:21; 1Nya 23:32; 2Nya 13:10
[p]**2:2** Za 74:4; Isa 31:9; Yer 4:21
[q]**2:3** Hes 6:23; Rut 4:20; 1Nya 2:10; Lk 3:32-33; Hes 10:14

Aminadabu. 4 Kundi lake lina watu
74,600.
5 [a]Kabila la Isakari watapiga kambi
karibu na Yuda. Kiongozi wa watu wa
Isakari ni Nethaneli mwana wa Suari.
6 [b]Kundi lake lina watu 54,400.
7 [c]Kabila la Zabuloni litafuata.
Kiongozi wa watu wa Zabuloni ni
Eliabu mwana wa Heloni. 8 Kundi lake
lina watu 57,400.
9 [d]Wanaume wote walio katika kambi
ya Yuda, kufuatana na makundi yao, ni
186,400. Wao watatangulia kuondoka.

10 [e]Kwa upande wa kusini kutakuwa
kambi ya makundi ya Reubeni chini
ya alama yao. Kiongozi wa watu wa
Reubeni ni Elisuri mwana wa Shedeuri.
11 Kundi lake lina watu 46,500.
12 [f]Kabila la Simeoni watapiga kambi
karibu na Reubeni. Kiongozi wa watu
wa Simeoni ni Shelumieli mwana wa
Surishadai. 13 Kundi lake lina watu
59,300.
14 [g]Kabila la Gadi litafuata. Kiongozi
wa watu wa Gadi ni Eliasafu mwana
wa Deueli. 15 Kundi lake lina watu
45,650.
16 [h]Wanaume wote walio katika
kambi ya Reubeni, kufuatana na
makundi yao, ni 151,450. Nao
watakuwa nafasi ya pili kuondoka.

17 [i]Kisha Hema la Kukutania na
kambi ya Walawi vitakuwa katikati
ya kambi zote. Wao watasafiri kwa
utaratibu ule ule kama walivyopiga
kambi, kila mmoja mahali pake
mwenyewe chini ya alama yake.

18 [j]Upande wa magharibi
kutakuwepo na kambi ya makundi ya
Efraimu chini ya alama yao. Kiongozi
wa watu wa Efraimu ni Elishama
mwana wa Amihudi. 19 Kundi lake lina
watu 40,500.
20 [k]Kabila la Manase litafuata
baada ya Efraimu. Kiongozi wa watu
wa Manase ni Gamalieli mwana wa
Pedasuri. 21 Kundi lake lina watu
32,200.
22 [l]Kabila la Benyamini litafuata
baada ya Manase. Kiongozi wa watu
wa Benyamini ni Abidani mwana
wa Gideoni. 23 Kundi lake lina watu
35,400.
24 [m]Wanaume wote walio katika kambi
ya Efraimu kufuatana na makundi yao
ni 108,100. Nao watakuwa nafasi ya
tatu kuondoka.

25 [n]Upande wa kaskazini kutakuwa
na makundi ya kambi ya Dani, chini
ya alama yao. Kiongozi wa watu wa
Dani ni Ahiezeri mwana wa Amishadai.
26 Kundi lake lina watu 62,700.
27 [o]Kabila la Asheri watapiga kambi
karibu na Dani. Kiongozi wa watu wa
Asheri ni Pagieli mwana wa Okrani.
28 Kundi lake lina watu 41,500.
29 [p]Kabila la Naftali litafuata.
Kiongozi wa watu wa Naftali ni Ahira
mwana wa Enani. 30 Kundi lake lina
watu 53,400.
31 [q]Wanaume wote walio katika
kambi ya Dani ni 157,600. Wao
watakuwa wa mwisho kuondoka chini
ya alama yao.

32 [r]Hawa ndio Waisraeli, wakiwa
wamehesabiwa kufuatana na jamaa

---

[a]**2:5** Hes 1:8; 10:15
[b]**2:6** Hes 26:25
[c]**2:7** Hes 1:9; 10:16; Mwa 49:13; Kum 33:18
[d]**2:9** Hes 10:14; Amu 1:1; 1Nya 5:2; Za 78:52
[e]**2:10** Hes 1:5, 53; Kum 33:6
[f]**2:12** Hes 10:19; 1:6
[g]**2:14** Hes 10:20; 1:14
[h]**2:16** Hes 10:18; Mwa 49:3
[i]**2:17** Hes 1:50; 10:21; Mdo 4:4; Ebr 8:2; 1Kor 14:40
[j]**2:18** Hes 1:10, 53; Mwa 48:20; Yer 31:18-20; Za 80:1; Hos 11:3
[k]**2:20** Mwa 48:20; Hes 1:10
[l]**2:22** Hes 10:24; 1:11; Za 68:27
[m]**2:24** Hes 10:22; Za 80:2
[n]**2:25** Hes 1:22, 53; 10:25; Kum 32:22
[o]**2:27** Hes 1:13; 10:26
[p]**2:29** Hes 1:15; 10:27; Mwa 30:8; 49:21; 2Fal 15:29
[q]**2:31** Hes 10:25; Yos 6:9
[r]**2:32** Hes 1:45; Kut 12:35-37; 38:26

zao. Wote walio kambini kwa makundi
yao ni watu 603,550. 33 [a]Hata hivyo,
Walawi hawakuhesabiwa pamoja na
Waisraeli wengine, kama BWANA
alivyomwagiza Mose.

34 [b]Kwa hiyo Waisraeli wakafanya kila
kitu BWANA alichomwamuru Mose. Hivyo
ndivyo walivyopiga kambi chini ya alama
zao, pia hivyo ndivyo walivyoondoka, kila
mmoja akiwa na ukoo wake na jamaa yake.

*Walawi*

3 [c]Hii ni hesabu ya jamaa ya Aroni na Mose
kwa wakati ambao BWANA alizungumza
na Mose katika Mlima Sinai.

2 [d]Majina ya wana wa Aroni yalikuwa:
Nadabu mzaliwa wa kwanza na Abihu,
Eleazari na Ithamari. 3 [e]Hayo yalikuwa
majina ya wana wa Aroni, makuhani
wapakwa mafuta, waliokuwa wamesimikwa
kuhudumu kama makuhani. 4 [f]Hata
hivyo Nadabu na Abihu walikufa mbele
za BWANA walipotoa sadaka kwa moto
usioruhusiwa mbele zake katika Jangwa
la Sinai. Hawakuwa na wana; kwa hiyo
Eleazari na Ithamari walihudumu peke yao
kama makuhani wakati wote wa maisha ya
Aroni baba yao.
5 BWANA akamwambia Mose, 6 [g]"Walete
watu wa kabila la Lawi mbele ya Aroni
kuhani ili wamsaidie. 7 [h]Watafanya huduma
kwa ajili yake na kwa jumuiya yote katika
Hema la Kukutania kwa kufanya kazi
za Maskani. 8 Watatunza samani zote za
Hema la Kukutania, wakitimiza wajibu
wa kuhudumia Waisraeli kwa kufanya
kazi ya Maskani. 9 [i]Wakabidhi Walawi
kwa Aroni na wanawe; hao ndio Waisraeli
ambao wanakabidhiwa kwake kabisa.
10 [j]Waweke Aroni na wanawe kuhudumu
kama makuhani; mtu mwingine yeyote
atakayesogea mahali patakatifu ni lazima
auawe."
11 BWANA akamwambia Mose,
12 [k]"Nimewatwaa Walawi kutoka miongoni
mwa Waisraeli badala ya mzaliwa wa
kwanza wa kiume wa kila mwanamke
wa Mwisraeli. Walawi ni wangu, 13 [l]kwa
kuwa wazaliwa wote wa kwanza ni
wangu. Nilipowaua wazaliwa wa kwanza
huko Misri, nilimtenga kila mzaliwa wa
kwanza katika Israeli awe wangu, akiwa
mwanadamu au mnyama. Watakuwa
wangu. Mimi ndimi BWANA."
14 BWANA akamwambia Mose katika
Jangwa la Sinai, 15 [m]"Wahesabu Walawi
kwa jamaa zao na koo zao. Mhesabu kila
mwanaume mwenye umri wa mwezi mmoja
au zaidi." 16 Kwa hiyo Mose akawahesabu,
kama alivyoamriwa na neno la BWANA.

17 [n]Haya yalikuwa majina ya wana wa
Lawi:
Gershoni, Kohathi na Merari.
18 [o]Haya ndiyo yaliyokuwa majina ya
koo za Wagershoni:
Libni na Shimei.
19 [p]Koo za Wakohathi zilikuwa ni:
Amramu, Ishari, Hebroni na
Uzieli.
20 [q]Koo za Wamerari zilikuwa ni:
Mahli na Mushi.

Hizi ndizo zilizokuwa koo za Walawi,
kufuatana na jamaa zao.

21 [r]Kulikuwa na koo za Walibni na
Washimei kwa Gershoni; hizi ndizo

[a]**2:33** Hes 1:47; 26:57-62
[b]**2:34** Kut 12:37; Hes 24:2, 9; Isa 45:12
[c]**3:1** Kut 6:27; 19:11
[d]**3:2** Hes 1:20; 26:30; Kut 6:23; 1Nya 6:3
[e]**3:3** Kut 28:41; 29:30
[f]**3:4** Law 10:1-6, 12; Hes 4:28; 1Nya 24:1; Hes 26:61; Kum 4:24; Isa 66:15; 2The 1:8; Ebr 12:29
[g]**3:6** Kum 10:8; 31:9; 1Nya 15:2; Hes 8:6-22; 18:1-7; 2Nya 29:11
[h]**3:7** Hes 1:53; 8:19; Law 8:35
[i]**3:9** Hes 8:19; 18:6
[j]**3:10** Kut 30:7; 29:9; Hes 1:51; 18:7; Mdo 6:3-4; Rum 12:7; 1Sam 6:19; Hes 16:40; 18:7
[k]**3:12** Neh 13:12; Mal 2:4; Hes 8:14, 16-18; 16:9; Kut 13:2
[l]**3:13** Kut 13:12; Law 11:44
[m]**3:15** Hes 1:19; 18:16; 26:62
[n]**3:17** Mwa 29:34; 46:11; Hes 1:47; 1Nya 15:4; 23:6; 2Nya 29:12; Yos 21:4-6
[o]**3:18** Kut 6:16-17
[p]**3:19** Kut 6:18
[q]**3:20** Mwa 46:11; Kut 6:19
[r]**3:21** Mwa 46:11; Kut 6:17

zilizokuwa koo za Wagershoni. 22 Idadi ya waume wote waliokuwa na mwezi mmoja au zaidi waliohesabiwa walikuwa 7,500. 23 [a]Ukoo wa Wagershoni walitakiwa kuweka kambi zao upande wa magharibi, nyuma ya Maskani. 24 Kiongozi wa jamaa za Wagershoni alikuwa Eliasafu mwana wa Laeli. 25 [b]Katika Hema la Kukutania, Wagershoni walikuwa na wajibu wa kutunza Maskani na hema, vifuniko vyake, pazia katika mlango wa kuingilia ndani ya Hema la Kukutania, 26 [c]mapazia ya ua, pazia katika ingilio la ua unaozunguka Maskani na madhabahu, pamoja na kamba, na kila kinachohusika kwa matumizi yake.

27 [d]Kwa Kohathi kulikuwepo koo za Waamramu, Waishari, Wahebroni na Wauzieli; hizi ndizo zilizokuwa koo za Wakohathi. 28 [e]Hesabu ya waume wote wenye mwezi mmoja au zaidi ilikuwa watu 8,600. Wakohathi waliwajibika kutunza mahali patakatifu. 29 [f]Koo za Wakohathi zilitakiwa kuweka kambi zao upande wa kusini wa Maskani. 30 [g]Kiongozi wa jamaa za koo za Wakohathi alikuwa Elisafani mwana wa Uzieli. 31 [h]Waliwajibika kutunza Sanduku la Agano, meza, kinara cha taa, madhabahu, na vile vyombo vya mahali patakatifu vinavyotumika kuhudumu, pazia, na kila kitu kinachohusika na matumizi yake. 32 [i]Kiongozi mkuu wa Walawi alikuwa Eleazari mwana wa kuhani, Aroni. Aliwekwa juu ya wale waliowajibika kutunza mahali patakatifu.

33 [j]Kwa Merari kulikuwa na koo za Wamahli na Wamushi; hizi zilikuwa koo za Merari. 34 Hesabu ya waume wote wenye umri wa mwaka mmoja au zaidi waliohesabiwa walikuwa 6,200. 35 [k]Kiongozi wa jamaa za koo za Wamerari alikuwa Surieli mwana wa Abihaili; hawa walitakiwa kuweka kambi zao upande wa kaskazini mwa Maskani. 36 [l]Wamerari waliwekwa kutunza miimo ya Maskani, mataruma yake, nguzo, vitako na vifaa vyake vyote na kila kitu kilichohusika na matumizi yake, 37 [m]na pia nguzo za ua unaozunguka pamoja na vitako vyake, vigingi vya hema na kamba zake.

38 [n]Mose, na Aroni na wanawe walitakiwa kuweka kambi zao mashariki mwa Maskani, kuelekea mawio ya jua, mbele ya Hema la Kukutania. Wao walihusika na utunzaji wa mahali patakatifu kwa niaba ya Waisraeli. Mtu mwingine yeyote aliyepasogelea mahali patakatifu angeuawa.

39 [o]Jumla ya hesabu ya Walawi waliohesabiwa na Mose na Aroni kwa amri ya Bwana, kufuatana na koo, pamoja na kila mume mwenye umri wa mwezi mmoja au zaidi, walikuwa 22,000.

40 Bwana akamwambia Mose, “Wahesabu wazaliwa wa kwanza wa kiume wote wa Waisraeli wenye umri wa mwezi mmoja au zaidi na uorodheshe majina yao. 41 [p]Nitwalie Walawi badala ya wazaliwa wa kwanza wa Waisraeli, nayo mifugo ya Walawi badala ya wazaliwa wa mifugo ya Waisraeli. Mimi ndimi Bwana.”

42 Hivyo Mose akawahesabu wazaliwa wa kwanza wote wa Waisraeli, kama Bwana alivyomwamuru. 43 Jumla ya hesabu ya wazaliwa wa kwanza waume wenye umri wa mwezi mmoja au zaidi,

[a]**3:23** Hes 2:18
[b]**3:25** Kut 25:9; 26:14, 36; 40:2; Hes 7:1; 4:25; 1Nya 9:14-33; Ezr 8:28-30
[c]**3:26** Kut 27:9; 35:18; Hes 4:26
[d]**3:27** Mwa 46:11; Kut 6:18; 1Nya 26:23; Hes 4:15, 37
[e]**3:28** Hes 4:4, 15; Kut 25:8; 30:13; 2Nya 30:19; Za 15:1; 20:2; Eze 44:27
[f]**3:29** Hes 1:53
[g]**3:30** Kut 6:22
[h]**3:31** Kut 25:10-22, 23, 31; 26:33; Kum 10:1-8; 2Nya 5:2; Yer 3:16; 1Nya 28:15; Yer 52:19; Hes 1:50; 4:5, 15; 18:3
[i]**3:32** Kut 6:23; Hes 4:19; 18:3; 20:25-28; 2Fal 25:18
[j]**3:33** Kut 6:19; Mwa 46:11
[k]**3:35** Hes 1:53; 2:25
[l]**3:36** Hes 4:32; Kut 26:15-25; 35:20-29; 36:36; Hes 18:3
[m]**3:37** Kut 27:10-19
[n]**3:38** Hes 2:3; 18:5; 1:51; 1Nya 9:27; 23:32
[o]**3:39** Hes 26:62
[p]**3:41** Law 11:44

walioorodheshwa kwa majina, walikuwa
22,273.
44 Bwana akamwambia Mose,
45 [a]"Watwae Walawi badala ya wazaliwa
wa kwanza wote wa Israeli, nayo mifugo
ya Walawi badala ya mifugo yao. Walawi
watakuwa wangu. Mimi ndimi Bwana.
46 [b]Ili kukomboa wazao wa kwanza 273
wa Waisraeli ambao wamezidi hesabu ya
Walawi, 47 [c]kusanya shekeli tano[d] kwa kila
mmoja, kufuatana na shekeli ya mahali
patakatifu, ambayo ina uzito wa gera
ishirini.[e] 48 Mpe Aroni na wanawe hizo
fedha kwa ajili ya ukombozi wa idadi ya
Waisraeli waliozidi."
49 [f]Kwa hiyo Mose akakusanya fedha
za ukombozi kutoka kwa wale ambao
hesabu yao ilizidi wale waliokombolewa
na Walawi. 50 [g]Kutokana na wazaliwa wa
kwanza wa Waisraeli alikusanya fedha
yenye uzito wa shekeli 1,365[h] kufuatana
na shekeli ya mahali patakatifu. 51 Mose
akampa Aroni na wanawe ile fedha ya
ukombozi, kama alivyoamriwa na neno la
Bwana.

*Wakohathi*

4 Bwana akawaambia Mose na Aroni,
2 [i]"Wahesabu Wakohathi walio sehemu
ya Walawi kwa koo zao na jamaa zao.
3 [j]Wahesabu wanaume wote wenye umri wa
miaka thelathini hadi hamsini wanaokuja
kutumika katika kazi ya Hema la Kukutania.
4 [k]"Hii ndiyo kazi ya Wakohathi katika
Hema la Kukutania: Watatunza vitu
vilivyo vitakatifu sana. 5 [l]Wakati kambi
inapohamishwa, Aroni na wanawe
wataingia ndani na kushusha lile pazia
la kuzuilia na kufunika nalo Sanduku la
Ushuhuda. 6 [m]Kisha watafunika juu yake na
ngozi za pomboo,[n] na kutandaza juu yake
kitambaa cha rangi ya buluu iliyokolea na
kuingiza mipiko mahali pake.
7 [o]"Juu ya meza ya mikate ya Wonyesho
watatandaza kitambaa cha buluu na
waweke sahani juu yake, masinia, bakuli na
magudulia kwa ajili ya sadaka za kinywaji;
mkate ule ambao upo hapa daima utabaki
juu yake. 8 [p]Juu ya hivyo vitu watatandaza
kitambaa chekundu na kufunika kwa ngozi
za pomboo na kuweka mipiko yake mahali
pake.
9 [q]"Watachukua kitambaa cha buluu na
kufunika kinara cha taa kilicho kwa ajili ya
nuru, pamoja na taa zake, mikasi yake, sinia
zake, magudulia yake yote yaliyotumika
kuwekea mafuta. 10 Kisha watakisokotea
pamoja na vifaa vyake vyote katika ngozi za
pomboo na kukiweka kwenye jukwaa lake.
11 [r]"Juu ya madhabahu ya dhahabu
watatandaza kitambaa cha buluu na
kukifunika kwa ngozi za pomboo na kuweka
mipiko yake mahali pake.
12 [s]"Watavichukua vyombo vyote
vinavyotumika kuhudumia mahali
patakatifu, watavisokotea kwenye
kitambaa cha buluu na kufunika kwa ngozi
za pomboo, na kuviweka juu ya miti ya
kuchukulia.
13 [t]"Wataondoa majivu kutoka madhabahu
ya shaba na kutandaza kitambaa cha
zambarau juu yake. 14 [u]Kisha wataweka

[a]**3:45** Hes 3:12; 1Sam 1:28
[b]**3:46** Kut 13:13; Hes 18:15
[c]**3:47** Law 27:6, 25; Kut 30:13; Hes 18:16; Eze 45:12
[d]47 Shekeli tano ni sawa na gramu 55.
[e]47 Gera 20 ni sawa na gramu 11.
[f]**3:49** 1Tim 2:6; Tit 2:14; Gal 4:4-5; 1Pet 1:18; Ebr 9:12
[g]**3:50** 1Sam 12:3-4; Mdo 20:33
[h]50 Shekeli 1,365 ni sawa na kilo 15.5.
[i]**4:2** Kut 30:12
[j]**4:3** Hes 1:46; 8:25; 1Nya 23:3, 24-27; Mwa 41:46; Ezr 3:8; Lk 3:23
[k]**4:4** Hes 3:28; 7:9
[l]**4:5** Kut 25:10, 16; 26:31-33; 1Nya 23:26; Law 16:2; 2Nya 3:14; Mt 27:51
[m]**4:6** Kut 25:5, 13-15; 1Fal 8:7; 2Nya 5:8
[n]6 *Pomboo* hapa ina maana ya mnyama mwenye ngozi laini aishiye kwenye milima yenye misitu, au pengine nguva au sili.
[o]**4:7** Law 24:6; Kut 25:30; 39:36; Yer 52:19
[p]**4:8** Kut 26:26-28
[q]**4:9** Kut 25:38
[r]**4:11** Kut 30:1-4
[s]**4:12** Hes 3:31
[t]**4:13** Law 1:16; Kut 27:1-8; Hes 3:31
[u]**4:14** Kut 31:9; 27:3, 6; 1Nya 28:17; 2Nya 4:8, 11-16; Hes 7:84; Yer 52:6

vyombo vyote juu yake vinavyotumika
kwa kuhudumia madhabahuni pamoja na
vyombo vya kutolea moto, nyuma, miiko
na mabakuli ya kunyunyizia. Juu yake
watatandaza ngozi za pomboo ya kufunika,
na kuweka mipiko mahali pake.
15 [a]“Baada ya Aroni na wanawe kumaliza
kazi ya kufunika samani takatifu na vyombo
vyake vyote, watu watakapokuwa tayari
kung’oa kambi, Wakohathi watakuja
kufanya kazi ya kubeba. Lakini wasije
wakagusa vitu vitakatifu la sivyo watakufa.
Wakohathi ndio watakaobeba vile vitu
vilivyomo katika Hema la Kukutania.
16 [b]“Eleazari mwana wa Aroni, kuhani,
ndiye atakayesimamia mafuta kwa ajili ya
taa, uvumba wenye harufu nzuri, sadaka
za kila siku za nafaka na mafuta ya upako.
Ndiye atakayekuwa msimamizi wa maskani
yote ya Bwana na kila kitu kilichomo
ndani mwake pamoja na samani takatifu
na vyombo vyake.”
17 Bwana akawaambia Mose na Aroni,
18 “Hakikisheni kwamba koo za kabila la
Wakohathi hawatengwi kutoka Walawi. 19 [c]Ili
wapate kuishi wala wasife wanapokaribia
vitu vitakatifu sana, uwafanyie hivi: Aroni
na wanawe watakwenda mahali patakatifu
na kumgawia kila mtu kazi yake, na
kwamba ni nini atakachochukua. 20 [d]Lakini
Wakohathi hawaruhusiwi kuingia ndani ili
kuangalia vitu vitakatifu, hata kwa kitambo
kidogo, la sivyo watakufa.”

*Wagershoni*

21 Bwana akamwambia Mose,
22 “Wahesabu pia Wagershoni kwa jamaa
zao na koo zao. 23 [e]Wahesabu wanaume
wote wenye umri wa miaka thelathini hadi
hamsini ambao huja kutumika katika Hema
la Kukutania.
24 “Hii ndiyo huduma ya koo za
Wagershoni wakati wanapofanya kazi na
kubeba mizigo. 25 [f]Watabeba mapazia ya
maskani. Hema la Kukutania, kifuniko
chake na kifuniko cha nje cha ngozi za
pomboo, mapazia ya maingilio ya Hema la
Kukutania, 26 [g]mapazia ya ua unaozunguka
Maskani na madhabahu, pazia la maingilio,
kamba na vifaa vyote vinavyotumika katika
huduma yake. Wagershoni watafanya
yote yatakiwayo kufanyika na vitu hivi.
27 Utumishi wao wote ukiwa ni kuchukua
au wa kufanya kazi nyingine, utafanyika
chini ya maelekezo ya Aroni na wanawe.
Mtawapangia kama wajibu wao yote
watakayoyafanya. 28 [h]Hii ndiyo huduma
ya koo za Wagershoni katika Hema la
Kukutania. Wajibu wao utakuwa chini ya
maelekezo ya Ithamari mwana wa kuhani
Aroni.

*Wamerari*

29 [i]“Wahesabu Wamerari kwa koo zao
na jamaa zao. 30 Wahesabu wanaume wote
kuanzia umri wa miaka thelathini hadi
hamsini ambao watakuja kutumika katika
Hema la Kukutania. 31 [j]Huu ndio wajibu
wao wanapofanya huduma katika Hema
la Kukutania: kubeba miimo ya Maskani,
mataruma yake, nguzo na vitako, 32 [k]nguzo
za ua unaozunguka pamoja na vitako vyake,
vigingi vya hema, kamba, vifaa vyake vyote
na kila kitu kinachohusiana na matumizi
yake. Kila mtu mpangie vitu maalum vya
kubeba. 33 [l]Huu ndio utumishi wa koo za
Merari kama watakavyofanya kazi katika
Hema la Kukutania, chini ya maelekezo ya
Ithamari mwana wa kuhani, Aroni.”

*Kuhesabiwa Kwa Koo Za Walawi*

34 [m]Mose, Aroni na viongozi wa jumuiya
wakawahesabu Wakohathi kwa koo zao

---

[a]**4:15** Hes 3:27; 7:9; Kut 28:43; Hes 1:51; 2Sam 6:6, 7; Kum 31:9; 2Sam 6:6-7, 13; 1Nya 28:12-13
[b]**4:16** Law 6:14-23; 10:6; Hes 3:32; Kut 25:6; 29:41
[c]**4:19** Hes 3:32
[d]**4:20** Kut 19:21; 1Sam 6:19
[e]**4:23** Hes 4:3; 1Nya 23:3; 24:27
[f]**4:25** Kut 26:14; 27:10-18; Hes 3:25
[g]**4:26** Kut 27:9, 16; Hes 3:26
[h]**4:28** Hes 7:7; Kut 6:23
[i]**4:29** Kut 30:12; Mwa 46:11
[j]**4:31** Hes 3:36; Kut 26:15; 27:9-19
[k]**4:32** Hes 3:37; Kut 25:9; 1Nya 9:29; Ezr 8:24-30
[l]**4:33** Kut 28:21
[m]**4:34** Hes 4:35-40; 1Kor 12:8-12; Kum 33:25

na jamaa zao. 35 Wanaume wote kuanzia
umri wa miaka thelathini hadi hamsini
ambao walikuja kutumika katika Hema la
Kukutania, 36 waliohesabiwa kwa koo zao,
walikuwa 2,750. 37 [a]Hii ilikuwa ndiyo jumla
ya wote wale wa koo za Wakohathi ambao
walitumika katika Hema la Kukutania.
Mose na Aroni waliwahesabu kufuatana
na amri ya BWANA kupitia kwa Mose.

38 [b]Wagershoni walihesabiwa kwa koo
zao na jamaa zao. 39 Watu wote kuanzia
umri wa miaka thelathini hadi hamsini
ambao walikuja kutumika katika Hema
la Kukutania, 40 waliohesabiwa kwa koo
zao na jamaa zao, walikuwa 2,630. 41 Hii
ilikuwa ndiyo jumla ya wale wa koo za
Gershoni ambao walitumika katika Hema
la Kukutania. Mose na Aroni waliwahesabu
kufuatana na amri ya BWANA.

42 Wamerari walihesabiwa kwa koo zao
na jamaa zao. 43 Wanaume wote kuanzia
umri wa miaka thelathini hadi miaka
hamsini ambao walikuja kutumika katika
Hema la Kukutania, 44 waliohesabiwa kwa
koo zao, walikuwa 3,200. 45 Hii ilikuwa
ndiyo jumla ya wale wa koo za Wamerari.
Mose na Aroni waliwahesabu kufuatia amri
ya BWANA kupitia kwa Mose.

46 Hivyo Mose, Aroni na viongozi wa
Israeli waliwahesabu Walawi wote kwa koo
zao na jamaa zao. 47 [c]Wanaume wote wenye
umri kuanzia miaka thelathini hadi hamsini
waliokuja kufanya kazi ya kuhudumu na
kubeba Hema la Kukutania 48 [d]walikuwa
watu 8,580. 49 [e]Kwa amri ya BWANA kupitia
Mose, kila mmoja aligawiwa kazi yake na
kuambiwa kitu cha kubeba.

Hivyo ndivyo walivyohesabiwa kama
BWANA alivyomwamuru Mose.

[a]**4:37** Hes 3:27
[b]**4:38** Mwa 46:11
[c]**4:47** Rum 12:6-8
[d]**4:48** Hes 3:39
[e]**4:49** Hes 1:47; Rum 12:6-8

*Utakaso Wa Kambi*

5 BWANA akamwambia Mose, 2 [f]"Waamuru
Waisraeli kumtoa nje ya kambi mtu
yeyote ambaye ana ugonjwa wa ngozi
uambukizao,[g] au anayetokwa na majimaji
ya aina yoyote, au ambaye ni najisi kwa
utaratibu wa ibada kwa sababu ya maiti.
3 [h]Hii itakuwa ni kwa wote, yaani, wanaume
na wanawake; watoeni nje ya kambi ili
wasije wakanajisi kambi yao, ambamo
ninaishi miongoni mwao." 4 Waisraeli
wakafanya hivyo; wakawatoa nje ya kambi.
Wakafanya kama vile BWANA alivyokuwa
amemwelekeza Mose.

*Malipo Kwa Ajili Ya Makosa*

5 BWANA akamwambia Mose,
6 [i]"Waambie Waisraeli, 'Wakati mwanaume
au mwanamke akimkosea mwenzake
kwa njia yoyote, na kwa hivyo akawa
si mwaminifu kwa BWANA, mtu huyo
ana hatia, 7 [k]na ni lazima atubu dhambi
aliyoifanya. Ni lazima atoe malipo kamili
kwa ajili ya kosa lake, aongeze sehemu
ya tano juu ya malipo hayo na kutoa yote
kwa mtu aliyemkosea. 8 [l]Lakini ikiwa
mtu huyo hana jamaa ya karibu ambaye
malipo yanaweza kufanywa kwa ajili ya
kosa, malipo yatakuwa mali ya BWANA,
nayo ni lazima apewe kuhani, pamoja na
kondoo dume ambaye anatumika kufanyia
upatanisho kwa ajili yake. 9 [m]Matoleo yote
matakatifu ya Waisraeli wanayoleta kwa
kuhani yatakuwa yake. 10 [n]Kila kitu cha mtu
kilichowekwa wakfu ni chake mwenyewe,
lakini kile atoacho kwa kuhani kitakuwa
cha kuhani.' "

[f]**5:2** Law 13:2, 3; 15:2; 21:11; Mt 9:20; Hes 9:6-10; 12:14; Kum 23:10; 2Fal 5:27; 2Nya 26:20; Isa 52:11; Lk 17:12
[g]2 Ugonjwa wa ngozi uambukizao hapa ina maana ya ukoma.
[h]**5:3** Kut 29:45; Law 26:12; 2Kor 6:16; Kut 25:8; Yos 22:19; Eze 37:26-28; Zek 2:10
[i]**5:6** Law 6:2; 5:14–6:7
[k]**5:7** Law 5:5, 16; 6:5; Lk 19:8; Yos 7:19
[l]**5:8** Law 5:15; 6:6-7
[m]**5:9** Law 6:17; 7:6-14; Kut 29:28
[n]**5:10** Law 7:29-34; 10:13

*Jaribio Kwa Ajili Ya Mke Asiye Mwaminifu*

11 Kisha BWANA akamwambia Mose,
12 [a]“Nena na Waisraeli uwaambie: ‘Ikiwa
mke wa mtu amepotoka na si mwaminifu
kwa mumewe, 13 [b]kwa kukutana kimwili na
mwanaume mwingine, tendo hili likafichika
kwa mumewe na unajisi wake usigundulike
(kwa kuwa hakuna ushahidi dhidi yake,
naye hakukamatwa katika tendo hilo),
14 [c]nazo hisia za wivu zikamjia mumewe na
kumshuku mkewe, naye mke yule ni najisi,
au mumewe ana wivu na akamshuku ingawa
si najisi, 15 [d]basi atampeleka mkewe kwa
kuhani. Huyo mume itampasa apeleke pia
sadaka ya unga wa shayiri kiasi cha sehemu
ya kumi ya efa[e] kwa niaba ya mkewe. Huyo
mwanaume kamwe asimimine mafuta juu
ya huo unga wala asiweke uvumba juu
yake, kwa sababu ni sadaka ya nafaka
kwa ajili ya wivu, sadaka ya ukumbusho
ili kukumbushia uovu.

16 [f]“ ‘Kuhani atamleta huyo mwanamke
na kumsimamisha mbele za BWANA.
17 Kisha kuhani atachukua sehemu ya maji
matakatifu ndani ya gudulia la udongo
na kuchanganya na baadhi ya vumbi
kutoka sakafu ya Maskani. 18 [g]Baada ya
kuhani kumsimamisha huyo mwanamke
mbele za BWANA, atazifungua nywele za
huyo mwanamke na kuweka sadaka ya
ukumbusho mikononi mwake, ile sadaka
ya nafaka kwa ajili ya wivu, huku kuhani
mwenyewe akishikilia yale maji machungu
yaletayo laana. 19 Kisha kuhani atamwapiza
huyo mwanamke, akimwambia, “Ikiwa
hakuna mwanaume mwingine aliyekutana
kimwili nawe, wala hujapotoka na kuwa
najisi wakati ukiwa umeolewa na mumeo,
maji haya machungu yaletayo laana na
yasikudhuru. 20 Lakini ikiwa umepotoka
wakati ukiwa umeolewa na mume wako
na umejinajisi mwenyewe kwa kukutana
kimwili na mwanaume mwingine asiyekuwa
mumeo”; 21 [h]hapa kuhani atamweka huyo
mwanamke chini ya laana ya kiapo
akisema: “BWANA na awafanye watu wako
wakulaani na kukukataa, wakati BWANA
atakapolifanya paja lako kupooza na tumbo
lako kuvimba. 22 [i]Maji haya yaletayo laana
na yaingie ndani ya mwili wako ili tumbo
lako livimbe na paja lako lipooze.”[j]

“ ‘Kisha mwanamke atasema, “Amen. Iwe
hivyo.”

23 [k]“ ‘Kuhani ataandika laana hizi
kwenye kitabu, kisha atazioshea laana
hizo kwenye yale maji machungu. 24 Kuhani
atamnywesha yule mwanamke yale maji
machungu yaletayo laana, nayo maji
haya yatamwingia na kumsababishia
maumivu makali. 25 [l]Kuhani atachukua
sadaka ya nafaka kwa ajili ya wivu kutoka
mikononi mwa huyo mwanamke, naye
ataipunga mbele za BWANA na kuileta
madhabahuni. 26 Kisha kuhani atachota
sadaka ya nafaka mkono uliojaa kama
sehemu ya kumbukumbu na kuiteketeza juu
ya madhabahu, baada ya hayo, atamtaka
huyo mwanamke anywe yale maji. 27 [m]Kama
amejitia unajisi na kukosa uaminifu kwa
mumewe, wakati anapotakiwa anywe
maji yale yaletayo laana, yatamwingia
na kusababisha maumivu makali; tumbo
lake litavimba na paja lake litapooza,
naye atakuwa amelaaniwa miongoni mwa
watu wake. 28 [n]Hata hivyo, ikiwa huyo
mwanamke hakujitia unajisi, naye ni safi,
atasafishwa hatia na ataweza kuzaa watoto.

29 “ ‘Basi, hii ndiyo sheria ya wivu
mwanamke anapopotoka na kujitia unajisi
akiwa ameolewa na mumewe, 30 au hisia za
wivu zinapomjia mwanaume kwa sababu ya

---

[a]**5:12** Kut 20:14; Mit 2:16; 7:10-27; Hos 4:13
[b]**5:13** Kut 20:14; Law 18:20; 18:20; 20:10; Mit 30:20
[c]**5:14** Mit 6:34; 27:4; Wim 8:6; Isa 19:14
[d]**5:15** Kut 16:36; Law 6:20; Eze 21:23; 29:16; Law 5:11; 1Fal 17:18
[e]15 Sehemu ya kumi ya efa ni sawa na kilo moja.
[f]**5:16** Yer 17:10; 1Nya 28:9; Ebr 13:4
[g]**5:18** Law 10:6; 1Kor 11:6
[h]**5:21** Yos 6:26; 1Sam 14:24; Neh 10:29; Mwa 9:25; Isa 65:15; Yer 29:22
[i]**5:22** Za 109:18; Kum 27:15
[j]22 Paja lipooze hapa ina maana ya kuwa tasa au kuharibu mimba.
[k]**5:23** Yer 45:1
[l]**5:25** Law 8:27; Kum 29:24
[m]**5:27** Isa 43:28; 65:15; Yer 26:6; 29:18; 42:18; 44:12, 22; Zek 8:13
[n]**5:28** Ay 17:8-9; Za 47:5-6; Rum 5:3-5

kumshuku mkewe. Kuhani atamfanya huyo
mwanamke kusimama mbele za BWANA
na atatumia sheria hii yote kwa huyo
mwanamke. [31] [a]Mume atakuwa hana hatia
ya kosa lolote, bali mwanamke atayachukua
matokeo ya dhambi yake.' "

*Mnadhiri*

6 BWANA akamwambia Mose, [2] [b]"Sema
na Waisraeli na uwaambie: 'Ikiwa
mwanaume au mwanamke anataka kuweka
nadhiri maalum, nadhiri ya kutengwa
kwa ajili ya BWANA kama Mnadhiri, [3] [c]ni
lazima ajitenge na mvinyo na kinywaji
kingine chochote chenye chachu, na
kamwe asinywe siki itokanayo na mvinyo
au itokanayo na kinywaji kingine chenye
chachu. Kamwe asinywe maji ya zabibu
wala kula zabibu mbichi au kavu. [4] Kwa
muda wote atakaokuwa Mnadhiri, kamwe
hatakula chochote kitokanacho na mzabibu,
sio mbegu wala maganda.

[5] [d]" 'Kwa muda wote wa nadhiri yake
ya kujitenga kwa ajili ya BWANA, wembe
hautapita kichwani mwake. Ni lazima awe
mtakatifu mpaka kipindi cha kujitenga
kwake kwa ajili ya BWANA kiishe; ni lazima
aache nywele za kichwa chake zirefuke.
[6] [e]Kwa kipindi chochote cha kujitenga kwa
ajili ya BWANA hatakaribia maiti. [7] [f]Hata
kama baba yake mwenyewe au mama au
kaka au dada akifa, hatajinajisi mwenyewe
kwa taratibu za ibada kwa ajili yao, kwa
sababu ishara ya kujiweka wakfu kwake
kwa Mungu ipo katika kichwa chake. [8] Kwa
kipindi chote cha kujitenga kwake yeye ni
wakfu kwa BWANA.

[9] [g]" 'Kama mtu yeyote akifa ghafula karibu
naye, atakuwa ametiwa unajisi nywele zake
alizoziweka wakfu, hivyo ni lazima anyoe
nywele zake siku ya utakaso wake, yaani
siku ya saba. [10] [h]Kisha siku ya nane ni lazima
alete hua wawili au makinda mawili ya
njiwa kwa kuhani katika mlango wa Hema
la Kukutania. [11] [i]Kuhani atatoa mmoja
kama sadaka ya dhambi, na mwingine
kama sadaka ya kuteketezwa ili kufanya
upatanisho kwa ajili yake kwa sababu
ametenda dhambi kwa kuwepo mbele
ya maiti. Siku iyo hiyo atakiweka wakfu
kichwa chake. [12] [j]Ni lazima ajitoe kabisa
kwa BWANA kwa kipindi cha kujitenga
kwake, na ni lazima atoe mwana-kondoo
wa mwaka mmoja kama sadaka ya hatia.
Siku zilizopita hazitahesabiwa kwa sababu
alijitia unajisi katika siku zake za kujitenga.

[13] [k]" 'Basi hii ndiyo sheria kwa ajili ya
Mnadhiri baada ya kipindi chake cha
kujitenga kupita. Ataletwa kwenye ingilio
la Hema la Kukutania. [14] [l]Hapo atatoa
sadaka zake kwa BWANA: yaani, mwana-
kondoo wa mwaka mmoja asiye na waa
kwa ajili ya sadaka ya kuteketezwa, kondoo
mke wa mwaka mmoja asiye na waa kwa
ajili ya sadaka ya dhambi, kondoo dume
asiye na waa kwa ajili ya sadaka ya amani,
[15] [m]pamoja na sadaka zake za nafaka na za
vinywaji, na kikapu cha mikate isiyotiwa
chachu, yaani maandazi yaliyotengenezwa
kwa unga laini uliochanganywa na mafuta,
na mikate myembamba iliyopakwa mafuta.

[16] " 'Kuhani atavileta vitu hivyo mbele
za BWANA na kufanya sadaka ya dhambi
na sadaka ya kuteketezwa. [17] [n]Ataleta pia
kikapu cha mikate isiyotiwa chachu, na
atatoa dhabihu kondoo dume kama sadaka
ya amani kwa BWANA, pamoja na sadaka
yake ya nafaka na sadaka ya kinywaji.

---

[a]**5:31** Law 5:1; 20:17; Eze 18:4; Rum 2:8-9
[b]**6:2** Hes 6:5, 6; Mwa 28:20; Mdo 21:23; Amu 13:5; 16:17
[c]**6:3** Law 10:9; 25:5; Lk 1:15; Rut 2:14; Za 69:21; Mit 10:26
[d]**6:5** Za 52:2; 57:4; 59:7; Isa 7:20; Eze 5:1; 1Sam 1:11; Mao 4:7
[e]**6:6** Law 21:1-3; Hes 19:11-22; Law 19:28; Yer 16:5-6; Eze 24:18; Mt 8:21
[f]**6:7** Hes 9:6
[g]**6:9** Law 14:9; Hes 6:18
[h]**6:10** Law 14:10-11; 5:7; 14:22
[i]**6:11** Kut 29:36; 30:10; Mwa 8:20
[j]**6:12** Law 12:6; 5:15
[k]**6:13** Mdo 21:26; Law 14:11
[l]**6:14** Kut 12:5; Law 4:3; 14:10; 5:15; 3:1
[m]**6:15** Law 2:1; 6:14; Mwa 35:14; Kut 29:2; Hes 15:1-7; Yn 6:50-53; Isa 62:9; 1Kor 10:31; 11:26
[n]**6:17** Kut 29:41; Law 23:13

18 [a]“ ‘Kisha kwenye ingilio la Hema la
Kukutania, Mnadhiri ni lazima anyoe
nywele zake ambazo alikuwa ameziweka
wakfu. Atazichukua hizo nywele na
kuziweka ndani ya moto ulio chini ya
dhabihu ya sadaka ya amani.
19 [b]“ ‘Baada ya Mnadhiri kunyoa hizo
nywele zake za kujitenga kwake, kuhani
atampa mikononi mwake bega la kondoo
dume lililochemshwa, na pia andazi
na mkate mwembamba kutoka kwenye
kikapu, vyote vikiwa vimetengenezwa
bila kuwekwa chachu. 20 [c]Kisha kuhani
ataviinua mbele za BWANA kama sadaka ya
kuinua; ni vitakatifu na ni mali ya kuhani,
pamoja na kile kidari kilichoinuliwa na lile
paja lililotolewa. Baada ya hayo, Mnadhiri
anaweza kunywa divai.
21 “ ‘Hii ndiyo sheria ya Mnadhiri ambaye
anaweka nadhiri kwa matoleo yake kwa
BWANA kufuatana na kujitenga kwake,
zaidi ya chochote kile anachoweza kupata.
Ni lazima atimize nadhiri aliyoiweka
kufuatana na sheria ya Mnadhiri.’ ”

*Baraka Ya Kikuhani*

22 BWANA akamwambia Mose,
23 [d]“Mwambie Aroni na wanawe, ‘Hivi
ndivyo mtakavyowabariki Waisraeli.
Waambieni:

24 [e]“ ‘ “BWANA akubariki
na kukulinda;
25 [f]BWANA akuangazie nuru ya uso
wake
na kukufadhili;
26 [g]BWANA akugeuzie uso wake
na kukupa amani.” ’

27 [h]“Hivyo wataliweka Jina langu juu ya
Waisraeli, nami nitawabariki.”

*Sadaka Wakati Wa Kuweka Wakfu Maskani Ya BWANA*

7 [i]Mose alipomaliza kuisimamisha
Maskani, aliitia mafuta na kuiweka
wakfu pamoja na samani zake zote. Pia
alitia madhabahu mafuta na kuiweka wakfu,
pamoja na vyombo vyake vyote. 2 [j]Ndipo
viongozi wa Israeli, wale wakuu wa jamaa
waliokuwa viongozi wa kabila wasimamizi
wa wale waliohesabiwa, wakatoa sadaka.
3 [k]Walizileta kama matoleo yao mbele
za BWANA: magari sita ya kukokotwa
yaliyofunikwa, pamoja na maksai kumi na
wawili; yaani maksai mmoja kutoka kwa
kila kiongozi, na gari moja la kukokotwa
kutoka kwa kila viongozi wawili. Haya
waliyaleta mbele ya Maskani.
4 BWANA akamwambia Mose, 5 “Vikubali
vitu hivi kutoka kwao, ili viweze kutumika
katika kazi kwenye Hema la Kukutania.
Wapatie Walawi kama kazi ya kila mtu
itakavyohitaji.”
6 Hivyo Mose akachukua yale magari ya
kukokotwa pamoja na maksai, na kuwapa
Walawi. 7 [l]Aliwapa Wagershoni magari
mawili ya kukokotwa na maksai wanne,
kama walivyohitaji kwa kazi yao, 8 [m]na
pia aliwapa Wamerari magari manne ya
kukokotwa na maksai wanane, kama kazi
yao ilivyohitaji. Wote walikuwa chini ya
maelekezo ya Ithamari mwana wa kuhani,
Aroni. 9 [n]Lakini Mose hakuwapa Wakohathi
chochote kati ya hivyo, kwa sababu
walitakiwa kubeba vitu vitakatifu mabegani
mwao, vile walikuwa wanawajibika.

---

[a]**6:18** Mdo 21:24; Lk 17:10; Rum 6:6; Gal 5:24; Efe 4:23; Kol 3:9
[b]**6:19** Law 7:12-13
[c]**6:20** Law 7:30; 27:9; 7:34; Mhu 9:7; Isa 35:10; Ufu 14:13
[d]**6:23** Kum 21:5; 1Nya 23:13
[e]**6:24** Mwa 28:3; Kum 28:3-6; Za 17:9; 28:9; 128:5; 1Sam 2:9
[f]**6:25** Ay 29:24; Za 4:6; 25:16; 86:16; 31:16; 80:3; 119:29, 135; Mwa 43:29
[g]**6:26** Za 4:6; 44:3; 4:8; 29:11; 37:11, 37; 127:2; Isa 14:7; Yer 33:6; Yn 14:27
[h]**6:27** Kum 28:10; 2Sam 7:23; Neh 9:10; Yer 25:29; Eze 36:23
[i]**7:1** Kut 40:9, 10, 17; 30:26; 2Nya 7:9; 1Fal 8:64
[j]**7:2** Hes 1:5-16, 19; Kut 35:27; 1Nya 29:6-8; Ezr 2:68-69; Neh 7:70-72
[k]**7:3** Mwa 45:19; 1Sam 6:7-14; 1Nya 13:6-7
[l]**7:7** Hes 4:24-28
[m]**7:8** Hes 4:31-33
[n]**7:9** Hes 4:4, 15; 1Nya 23:26; 2Sam 6:13

[10] [a]Wakati madhabahu yalitiwa mafuta, viongozi walileta sadaka zao kwa ajili ya kule kuwekwa wakfu kwake na kuziweka
mbele ya madhabahu. [11] [b]Kwa maana
Bwana alikuwa amemwambia Mose, "Kila siku kiongozi mmoja ataleta sadaka yake ili kuwekwa wakfu madhabahu."

[12] [c]Yule ambaye alileta sadaka yake siku ya kwanza alikuwa Nashoni, mwana wa Aminadabu, wa kabila la Yuda.

[13] [d]Sadaka yake ilikuwa sahani moja ya fedha yenye uzito wa shekeli 130,[e] na bakuli moja la fedha la kunyunyizia lenye uzito wa shekeli sabini,[f] vyote kulingana na shekeli ya mahali patakatifu, vikiwa vimejazwa unga laini uliochanganywa na mafuta
kama sadaka ya nafaka; [14] [g]sinia moja
la dhahabu lenye uzito wa shekeli kumi,[h] likiwa limejazwa uvumba;
[15] [i]fahali mmoja mchanga, kondoo dume mmoja na mwana-kondoo dume mmoja wa mwaka mmoja, kwa ajili
ya sadaka ya kuteketezwa; [16] [j]mbuzi
dume mmoja kwa ajili ya sadaka ya
dhambi; [17] [kl]maksai wawili, kondoo dume watano, mbuzi dume watano na wana-kondoo dume watano wa mwaka mmoja, ili vitolewe dhabihu kama sadaka ya amani. Hii ndiyo ilikuwa sadaka ya Nashoni mwana wa Aminadabu.

[18] [m]Siku ya pili yake Nethaneli mwana wa Suari, kiongozi wa kabila la Isakari, alileta sadaka yake.

[19] Sadaka aliyoleta ilikuwa sahani moja ya fedha yenye uzito wa shekeli 130, na bakuli moja la fedha la kunyunyizia lenye uzito wa shekeli sabini, vyote kulingana na shekeli ya mahali patakatifu, vikiwa vimejazwa unga laini uliochanganywa na mafuta
kama sadaka ya nafaka; [20] sinia moja
la dhahabu lenye uzito wa shekeli kumi, likiwa limejazwa uvumba;
[21] [n]fahali mmoja mchanga, kondoo dume mmoja na mwana-kondoo dume mmoja wa mwaka mmoja, kwa ajili
ya sadaka ya kuteketezwa; [22] mbuzi
dume mmoja kwa ajili ya sadaka ya
dhambi; [23] [o]maksai wawili, kondoo dume watano, mbuzi dume watano na wana-kondoo dume watano wa mwaka mmoja, ili vitolewe dhabihu kama sadaka ya amani. Hii ndiyo ilikuwa sadaka ya Nethaneli mwana wa Suari.

[24] [p]Siku ya tatu Eliabu mwana wa Heloni, kiongozi wa kabila la Zabuloni, alileta sadaka yake.

[25] [q]Sadaka aliyoleta ilikuwa sahani moja ya fedha yenye uzito wa shekeli 130, na bakuli moja la fedha la kunyunyizia lenye uzito wa shekeli sabini, vyote kulingana na shekeli ya mahali patakatifu, vikiwa vimejazwa unga laini uliochanganywa na mafuta
kama sadaka ya nafaka; [26] sinia moja
la dhahabu lenye uzito wa shekeli kumi, likiwa limejazwa uvumba;
[27] fahali mmoja mchanga, kondoo dume mmoja na mwana-kondoo dume mmoja wa mwaka mmoja, kwa ajili
ya sadaka ya kuteketezwa; [28] mbuzi
dume mmoja kwa ajili ya sadaka ya
dhambi; [29] maksai wawili, kondoo

---

[a]**7:10** Hes 7:1; Kut 29:36; 2Nya 7:9; Kum 20:5; Ezr 6:16
[b]**7:11** 1Kor 14:33
[c]**7:12** Hes 1:7
[d]**7:13** Kut 27:3; 30:13; Law 27:3-7; 2:1; Hes 6:15; 15:14; Ezr 8:25; Yer 52:19
[e]13 Shekeli 130 za fedha ni sawa na kilo 1.5.
[f]13 Shekeli 70 za fedha ni sawa gramu 800.
[g]**7:14** 1Fal 7:50; 2Fal 25:14; 2Nya 4:22; 24:14; Kut 25:6; 30:34; Eze 18:16; Mal 1:11; Ufu 5:8
[h]14 Shekeli 10 za dhahabu ni sawa na gramu 110.
[i]**7:15** Kut 24:5; 29:3; Hes 28:11; Law 1:3
[j]**7:16** Law 4:3
[k]**7:17** Law 3:1; Hes 1:7
[l]**7:17** Lk 3:32
[m]**7:18** Hes 1:8
[n]**7:21** Mwa 8:20; Za 20:1-3; 50:19; Efe 5:2; Ebr 9:13
[o]**7:23** 1Fal 8:63; Law 7:11-13; Mit 7:14; Kol 1:20
[p]**7:24** Hes 1:9
[q]**7:25** Isa 53:7; Mdo 8:32; Ufu 5:6-11; 13:8

dume watano, mbuzi dume watano na
wana-kondoo dume watano wa mwaka
mmoja, ili vitolewe dhabihu kama
sadaka ya amani. Hii ndiyo ilikuwa
sadaka ya Eliabu mwana wa Heloni.

30 [a]Siku ya nne Elisuri mwana wa Shedeuri,
kiongozi wa kabila la Reubeni, alileta
sadaka yake.

31 Sadaka aliyoleta ilikuwa sahani
moja ya fedha yenye uzito wa shekeli
130, na bakuli moja la fedha la
kunyunyizia lenye uzito wa shekeli
sabini, vyote kulingana na shekeli ya
mahali patakatifu, vikiwa vimejazwa
unga laini uliochanganywa na mafuta
kama sadaka ya nafaka; 32 sinia moja
la dhahabu lenye uzito wa shekeli
kumi, likiwa limejazwa uvumba;
33 fahali mmoja mchanga, kondoo
dume mmoja na mwana-kondoo dume
mmoja wa mwaka mmoja, kwa ajili
ya sadaka ya kuteketezwa; 34 mbuzi
dume mmoja kwa ajili ya sadaka ya
dhambi; 35 maksai wawili, kondoo
dume watano, mbuzi dume watano na
wana-kondoo dume watano wa mwaka
mmoja, ili vitolewe dhabihu kama
sadaka ya amani. Hii ndiyo ilikuwa
sadaka ya Elisuri mwana wa Shedeuri.

36 [b]Siku ya tano Shelumieli mwana wa
Surishadai, kiongozi wa watu wa Simeoni,
alileta sadaka yake.

37 Sadaka aliyoleta ilikuwa sahani
moja ya fedha yenye uzito wa shekeli
130, na bakuli moja la fedha la
kunyunyizia lenye uzito wa shekeli
sabini, vyote kulingana na shekeli ya
mahali patakatifu, vikiwa vimejazwa
unga laini uliochanganywa na mafuta
kama sadaka ya nafaka; 38 sinia moja
la dhahabu lenye uzito wa shekeli
kumi, likiwa limejazwa uvumba;
39 [c]fahali mmoja mchanga, kondoo
dume mmoja na mwana-kondoo dume
mmoja wa mwaka mmoja, kwa ajili
ya sadaka ya kuteketezwa; 40 mbuzi
dume mmoja kwa ajili ya sadaka ya
dhambi; 41 maksai wawili, kondoo
dume watano, mbuzi dume watano
na wana-kondoo dume watano wa
mwaka mmoja, ili vitolewe dhabihu
kama sadaka ya amani. Hii ndiyo
ilikuwa sadaka ya Shelumieli mwana
wa Surishadai.

42 [d]Siku ya sita Eliasafu mwana wa Deueli,
kiongozi wa watu wa Gadi, alileta sadaka
yake.

43 [e]Sadaka aliyoleta ilikuwa sahani
moja ya fedha yenye uzito wa shekeli
130, na bakuli moja la fedha la
kunyunyizia lenye uzito wa shekeli
sabini, vyote kulingana na shekeli ya
mahali patakatifu, vikiwa vimejazwa
unga laini uliochanganywa na mafuta
kama sadaka ya nafaka; 44 sinia moja
la dhahabu lenye uzito wa shekeli
kumi, likiwa limejazwa uvumba;
45 [f]fahali mmoja mchanga, kondoo
dume mmoja na mwana-kondoo dume
mmoja wa mwaka mmoja, kwa ajili
ya sadaka ya kuteketezwa; 46 mbuzi
dume mmoja kwa ajili ya sadaka ya
dhambi; 47 maksai wawili, kondoo
dume watano, mbuzi dume watano na
wana-kondoo dume watano wa mwaka
mmoja, ili vitolewe dhabihu kama
sadaka ya amani. Hii ndiyo ilikuwa
sadaka ya Eliasafu mwana wa Deueli.

48 [g]Siku ya saba Elishama mwana wa
Amihudi, kiongozi wa watu wa Efraimu,
alileta sadaka yake.

49 Sadaka aliyoleta ilikuwa sahani
moja ya fedha yenye uzito wa shekeli
130, na bakuli moja la fedha la
kunyunyizia lenye uzito wa shekeli
sabini, vyote kulingana na shekeli ya
mahali patakatifu, vikiwa vimejazwa
unga laini uliochanganywa na mafuta
kama sadaka ya nafaka; 50 [h]sinia moja

---

[a]**7:30** Hes 1:5
[b]**7:36** Hes 1:6
[c]**7:39** Kut 12:5; Ebr 9:28; 1Pet 3:18
[d]**7:42** Hes 1:14
[e]**7:43** Law 2:5; 14:10
[f]**7:45** Za 40:6; 51:16; Isa 53:4; Yer 7:22; Amo 5:22
[g]**7:48** Hes 1:10; 2:18; 1Nya 7:26
[h]**7:50** Kum 33:10; Za 66:15; Lk 1:10

la dhahabu lenye uzito wa shekeli
kumi, likiwa limejazwa uvumba;
51 [a]fahali mmoja mchanga, kondoo
dume mmoja na mwana-kondoo dume
mmoja wa mwaka mmoja, kwa ajili
ya sadaka ya kuteketezwa; 52 mbuzi
dume mmoja kwa ajili ya sadaka ya
dhambi; 53 maksai wawili, kondoo
dume watano, mbuzi dume watano
na wana-kondoo dume watano wa
mwaka mmoja, ili vitolewe dhabihu
kama sadaka ya amani. Hii ndiyo
ilikuwa sadaka ya Elishama mwana
wa Amihudi.

54 [b]Siku ya nane Gamalieli mwana wa
Pedasuri, kiongozi wa watu wa Manase,
alileta sadaka yake.
55 Sadaka aliyoleta ilikuwa sahani
moja ya fedha yenye uzito wa shekeli
130, na bakuli moja la fedha la
kunyunyizia lenye uzito wa shekeli
sabini, vyote kulingana na shekeli ya
mahali patakatifu, vikiwa vimejazwa
unga laini uliochanganywa na mafuta
kama sadaka ya nafaka; 56 [c]sinia moja
la dhahabu lenye uzito wa shekeli
kumi, likiwa limejazwa uvumba;
57 [d]fahali mmoja mchanga, kondoo
dume mmoja na mwana-kondoo dume
mmoja wa mwaka mmoja, kwa ajili
ya sadaka ya kuteketezwa; 58 mbuzi
dume mmoja kwa ajili ya sadaka ya
dhambi; 59 maksai wawili, kondoo
dume watano, mbuzi dume watano
na wana-kondoo dume watano wa
mwaka mmoja, ili vitolewe dhabihu
kama sadaka ya amani. Hii ndiyo
ilikuwa sadaka ya Gamalieli mwana
wa Pedasuri.

60 [e]Siku ya tisa Abidani mwana wa Gideoni,
kiongozi wa watu wa Benyamini, alileta
sadaka yake.
61 Sadaka aliyoleta ilikuwa sahani
moja ya fedha yenye uzito wa shekeli
130, na bakuli moja la fedha la
kunyunyizia lenye uzito wa shekeli
sabini, vyote kulingana na shekeli ya
mahali patakatifu, vikiwa vimejazwa
unga laini uliochanganywa na mafuta
kama sadaka ya nafaka; 62 [f]sinia moja
la dhahabu lenye uzito wa shekeli
kumi, likiwa limejazwa uvumba;
63 [g]fahali mmoja mchanga, kondoo
dume mmoja na mwana-kondoo dume
mmoja wa mwaka mmoja, kwa ajili
ya sadaka ya kuteketezwa; 64 mbuzi
dume mmoja kwa ajili ya sadaka ya
dhambi; 65 [h]maksai wawili, kondoo
dume watano, mbuzi dume watano na
wana-kondoo dume watano wa mwaka
mmoja, ili vitolewe dhabihu kama
sadaka ya amani. Hii ndiyo ilikuwa
sadaka ya Abidani mwana wa Gideoni.

66 [i]Siku ya kumi Ahiezeri mwana wa
Amishadai, kiongozi wa watu wa Dani,
alileta sadaka yake.
67 [j]Sadaka aliyoleta ilikuwa sahani
moja ya fedha yenye uzito wa shekeli
130, na bakuli moja la fedha la
kunyunyizia lenye uzito wa shekeli
sabini, vyote kulingana na shekeli ya
mahali patakatifu, vikiwa vimejazwa
unga laini uliochanganywa na mafuta
kama sadaka ya nafaka; 68 [k]sinia moja
la dhahabu lenye uzito wa shekeli
kumi, likiwa limejazwa uvumba;
69 fahali mmoja mchanga, kondoo
dume mmoja na mwana-kondoo dume
mmoja wa mwaka mmoja, kwa ajili
ya sadaka ya kuteketezwa; 70 mbuzi
dume mmoja kwa ajili ya sadaka ya
dhambi; 71 maksai wawili, kondoo
dume watano, mbuzi dume watano
na wana-kondoo dume watano wa
mwaka mmoja, ili vitolewe dhabihu
kama sadaka ya amani. Hii ndiyo

[a]**7:51** Mik 6:6-8
[b]**7:54** Hes 1:10
[c]**7:56** Kut 30:7
[d]**7:57** Kut 12:5; Mdo 8:32; 1Pet 1:19
[e]**7:60** Hes 1:11
[f]**7:62** Isa 66:20; Dan 9:27; Rum 15:16; Ebr 13:15; Ufu 8:3-4
[g]**7:63** Za 40:6; Isa 53:4; 2Kor 5:21
[h]**7:65** Mit 7:14; Eze 45:17; Kol 1:20
[i]**7:66** Hes 1:12; 2:25
[j]**7:67** Law 27:25; Hes 3:47; Kut 30:13
[k]**7:68** Hes 16:35; Za 141:2; Kut 30:7-9

ilikuwa sadaka ya Ahiezeri mwana
wa Amishadai.

72 [a]Siku ya kumi na moja Pagieli mwana
wa Okrani, kiongozi wa watu wa Asheri,
alileta sadaka yake.
73 Sadaka aliyoleta ilikuwa sahani
moja ya fedha yenye uzito wa shekeli
130, na bakuli moja la fedha la
kunyunyizia lenye uzito wa shekeli
sabini, vyote kulingana na shekeli ya
mahali patakatifu, vikiwa vimejazwa
unga laini uliochanganywa na mafuta
kama sadaka ya nafaka; 74 sinia moja
la dhahabu lenye uzito wa shekeli
kumi, likiwa limejazwa uvumba;
75 fahali mmoja mchanga, kondoo
dume mmoja na mwana-kondoo dume
mmoja wa mwaka mmoja, kwa ajili
ya sadaka ya kuteketezwa; 76 mbuzi
dume mmoja kwa ajili ya sadaka ya
dhambi; 77 maksai wawili, kondoo
dume watano, mbuzi dume watano na
wana-kondoo dume watano wa mwaka
mmoja, ili vitolewe dhabihu kama
sadaka ya amani. Hii ndiyo ilikuwa
sadaka ya Pagieli mwana wa Okrani.

78 [b]Siku ya kumi na mbili Ahira mwana wa
Enani, kiongozi wa watu wa Naftali, alileta
sadaka yake.
79 [c]Sadaka aliyoleta ilikuwa sahani
moja ya fedha yenye uzito wa shekeli
130, na bakuli moja la fedha la
kunyunyizia lenye uzito wa shekeli
sabini, vyote kulingana na shekeli ya
mahali patakatifu, vikiwa vimejazwa
unga laini uliochanganywa na mafuta
kama sadaka ya nafaka; 80 sinia moja
la dhahabu lenye uzito wa shekeli
kumi, likiwa limejazwa uvumba;
81 fahali mmoja mchanga, kondoo
dume mmoja na mwana-kondoo dume
mmoja wa mwaka mmoja, kwa ajili
ya sadaka ya kuteketezwa; 82 mbuzi
dume mmoja kwa ajili ya sadaka ya
dhambi; 83 maksai wawili, kondoo
dume watano, mbuzi dume watano na
wana-kondoo dume watano wa mwaka
mmoja, ili vitolewe dhabihu kama
sadaka ya amani. Hii ndiyo ilikuwa
sadaka ya Ahira mwana wa Enani.

84 [d]Hizi ndizo zilikuwa sadaka za viongozi
wa Israeli madhabahu yalipowekwa wakfu,
wakati yalitiwa mafuta: sahani kumi na
mbili za fedha, bakuli kumi na mbili za
fedha za kunyunyizia, na masinia kumi na
mawili ya dhahabu. 85 Kila sahani ya fedha
ilikuwa na uzito wa shekeli 130, na kila
bakuli la fedha la kunyunyizia lilikuwa na
uzito wa shekeli sabini. Masinia yote kumi
na mawili yalikuwa na uzito wa shekeli
2,400[e]kulingana na shekeli ya mahali
patakatifu. 86 [f]Sahani kumi na mbili za
dhahabu zilizojazwa uvumba zilikuwa
na uzito wa shekeli kumi kila moja,
kulingana na shekeli ya mahali patakatifu.
Kwa jumla, sahani za dhahabu zilikuwa
na uzito wa shekeli 120.[g] 87 Jumla ya
wanyama waliotolewa kwa ajili ya sadaka
ya kuteketezwa walikuwa fahali kumi na
wawili wachanga, kondoo dume kumi
na wawili na wana-kondoo dume kumi
na wawili wa mwaka mmoja, pamoja na
sadaka zao za nafaka. Mbuzi waume kumi
na wawili walitolewa kwa ajili ya sadaka
za dhambi. 88 [h]Jumla ya wanyama kwa ajili
ya dhabihu ya sadaka ya amani walikuwa
maksai ishirini na wanne, kondoo dume
sitini, mbuzi dume wa mwaka mmoja
sitini na wana-kondoo dume wa mwaka
mmoja sitini. Hizi ndizo zilikuwa sadaka
zilizoletwa kwa ajili ya kuwekwa wakfu
kwa madhabahu baada ya kutiwa mafuta.
89 [ij]Mose alipoingia kwenye Hema la
Kukutania kuzungumza na BWANA, alisikia
sauti ikisema naye kutoka kati ya wale

[a]**7:72** Hes 1:13
[b]**7:78** Hes 1:15; 2:29
[c]**7:79** Ezr 1:9-10; Yer 52:19; Zek 14:20; Mt 14:8-11
[d]**7:84** Hes 4:14; Neh 7:70; Ebr 13:10; Amu 5:9; Yos 22:13-14; Hos 13:10; Mit 17:7
[e]85 Shekeli 2,400 za fedha ni sawa na kilo 28.
[f]**7:86** Kut 30:13
[g]86 Shekeli 120 za dhahabu ni sawa na kilo 1.4.
[h]**7:88** Mwa 32:14
[i]**7:89** Kut 31:18; Hes 12:8; Ebr 4:16
[j]**7:89** Kut 25:22; 40:2; 29:42; 16:34; Za 80:1; 90:1; Hes 3:31

makerubi wawili waliokuwa juu ya kile kiti
cha rehema, juu ya Sanduku la Ushuhuda.
Mose akazungumza naye.

*Kuwekwa Kwa Taa*

8 BWANA akamwambia Mose, 2 [a]“Sema na
Aroni umwambie, ‘Wakati utakapoziweka
zile taa saba, zinatakiwa kuangaza eneo
lililo mbele ya kinara cha taa.’ ”
3 Aroni akafanya hivyo; akaziweka zile
taa ili zielekee mbele kwenye kinara cha
taa, kama vile BWANA alivyomwamuru
Mose. 4 [b]Hivi ndivyo kinara cha taa
kilivyotengenezwa: Kilitengenezwa kwa
dhahabu iliyofuliwa, kuanzia kwenye
kitako chake hadi kwenye maua yake.
Kinara cha taa kilitengenezwa sawasawa
kabisa na kielelezo ambacho BWANA
alikuwa amemwonyesha Mose.

*Kutengwa Kwa Walawi Kwa Ajili Ya BWANA*

5 BWANA akamwambia Mose: 6 [c]“Watwae
Walawi kutoka miongoni mwa Waisraeli
wengine na uwatakase kwa kawaida
ya ibada. 7 [d]Ili kuwatakasa fanya hivi:
Nyunyizia maji ya utakaso juu yao; kisha
uwaambie wanyoe nywele kwenye mwili
mzima, wafue nguo zao na hivyo wajitakase
wenyewe. 8 [e]Waambie wamchukue fahali
mchanga pamoja na sadaka yake ya nafaka
ya unga laini uliochanganywa na mafuta;
kisha utamchukua fahali mchanga wa pili
kwa ajili ya sadaka ya dhambi. 9 [f]Walete
Walawi mbele ya Hema la Kukutania
na ukusanye jumuiya yote ya Waisraeli.
10 [g]Utawaleta Walawi mbele za BWANA,
na Waisraeli wataweka mikono yao juu
ya Walawi. 11 [h]Aroni atawaweka Walawi
mbele za BWANA kama sadaka ya kuinua
kutoka kwa Waisraeli, ili kwamba wawe
tayari kuifanya kazi ya BWANA.
12 [i]“Baada ya Walawi kuweka mikono yao
juu ya vichwa vya hao mafahali wawili,
tumia mmoja kwa ajili ya sadaka ya dhambi
kwa BWANA, na mwingine kuwa sadaka ya
kuteketezwa, ili kufanya upatanisho kwa
ajili ya Walawi. 13 [j]Waambie hao Walawi
wasimame mbele ya Aroni na wanawe,
kisha wawatoe kama sadaka ya kuinuliwa
kwa BWANA. 14 [k]Kwa njia hii utakuwa
umewatenga Walawi kutoka kwa Waisraeli
wengine, nao Walawi watakuwa wangu.
15 [l]“Utakapokuwa umekwisha kuwatakasa
Walawi na kuwatoa kama sadaka ya
kuinuliwa, watakuja kufanya kazi yao
katika Hema la Kukutania. 16 [m]Wao ndio
Waisraeli ambao watatolewa kabisa
kwangu. Nimewatwaa kama mali yangu
mwenyewe badala ya mzaliwa wa kwanza,
mzaliwa wa kwanza wa kiume kutoka kwa
kila mwanamke wa Kiisraeli. 17 [n]Kila mzaliwa
wa kwanza wa kiume katika Israeli, awe wa
mwanadamu au mnyama, ni wangu. Wakati
nilipowaua wazaliwa wote wa kwanza
huko Misri, niliwatenga kwa ajili yangu
mwenyewe. 18 [o]Nami nimewatwaa Walawi
badala ya wazaliwa wote wa kwanza wa
kiume katika Israeli. 19 [p]Kati ya Waisraeli
wote, nimempa Aroni na wanawe Walawi
kama zawadi ili wafanye kazi katika Hema
la Kukutania kwa niaba ya Waisraeli,
na kufanya upatanisho kwa ajili yao ili
pasiwepo na pigo lolote litakalowapata
Waisraeli wakati watakapokaribia mahali
patakatifu.”
20 Mose, Aroni na jumuiya yote ya
Waisraeli wakawafanyia Walawi kama
BWANA alivyomwamuru Mose. 21 [q]Walawi
wakajitakasa wenyewe na wakafua nguo
zao. Kisha Aroni akawasogeza mbele

[a]**8:2** Kut 25:37; Law 24:2-4; Za 119:105; Isa 8:20; Mt 5:14
[b]**8:4** Kut 25:9, 36
[c]**8:6** Law 22:2; Isa 52:11; Za 26:6; Ebr 7:26; 10:22
[d]**8:7** Hes 19:9, 17; 31:23; Law 14:8, 9; Hes 6:9; Kum 21:21; Mwa 35:2
[e]**8:8** Law 2:1; 4:3; Hes 15:8-10
[f]**8:9** Kut 40:12; Law 8:3
[g]**8:10** Law 3:2; Mdo 6:6
[h]**8:11** Kut 29:24; Law 7:30
[i]**8:12** Kut 29:10, 36; Law 4:3; Hes 6:11
[j]**8:13** Kut 29:24
[k]**8:14** Hes 3:12; 3:45; 16:9; Mal 3:17
[l]**8:15** Kut 29:24; 40:2
[m]**8:16** Hes 1:20; 3:12
[n]**8:17** Kut 4:23; 22:29; 13:2; Lk 2:23
[o]**8:18** Hes 3:12
[p]**8:19** Hes 3:7-9; 1:53; 16:46; 18:2-6
[q]**8:21** Mwa 35:2; Rum 15:16

za BWANA kuwa sadaka ya kuinuliwa,
na kufanya upatanisho kwa ajili yao ili
kuwatakasa. 22 [a]Baada ya hayo, Walawi
walikuja kufanya kazi yao katika Hema la
Kukutania chini ya usimamizi wa Aroni na
wanawe. Waliwafanyia Walawi kama vile
BWANA alivyomwamuru Mose.
23 BWANA akamwambia Mose, 24 [b]"Hili
linawahusu Walawi: Wanaume wenye
umri wa miaka ishirini na mitano au zaidi
watakuja kushiriki katika kazi kwenye
Hema la Kukutania, 25 [c]lakini watakapofika
umri wa miaka hamsini, ni lazima waache
kazi zao za kawaida wala wasiendelee.
26 Wanaweza kuwasaidia ndugu zao kufanya
wajibu wao katika Hema la Kukutania,
lakini wao wenyewe kamwe hawatafanya
hiyo kazi. Basi, hivi ndivyo utakavyogawa
wajibu kwa Walawi."

*Pasaka Huko Sinai*

9 [d]BWANA akasema na Mose katika Jangwa
la Sinai katika mwezi wa kwanza wa
mwaka wa pili baada ya Waisraeli
kutoka Misri. Akasema, 2 [e]"Waamuru
Waisraeli waadhimishe Pasaka katika
wakati ulioamriwa. 3 [f]Adhimisheni wakati
ulioamriwa, yaani wakati wa kuzama
jua siku ya kumi na nne ya mwezi huu,
kufuatana na desturi zake zote na masharti
yake."
4 [g]Hivyo Mose akawaambia Waisraeli
waiadhimishe Pasaka, 5 [h]nao wakafanya
hivyo kwenye Jangwa la Sinai wakati wa
kuzama jua siku ya kumi na nne ya mwezi
wa kwanza. Waisraeli wakafanya kila kitu
kama vile BWANA alivyomwamuru Mose.
6 [i]Lakini baadhi yao hawakuweza
kuadhimisha Pasaka siku ile kwa sababu
walikuwa najisi kwa taratibu za kiibada
kwa ajili ya kugusa maiti. Kwa hiyo
wakamwendea Mose na Aroni siku ile ile,
7 wakamwambia Mose, "Tumekuwa najisi
kwa sababu tumegusa maiti, lakini kwa nini
tuzuiliwe kumtolea BWANA sadaka yake
pamoja na Waisraeli wengine katika wakati
ulioamriwa?"
8 [j]Mose akawajibu, "Ngojeni mpaka
nitafute kile BWANA anachoagiza kuwahusu
ninyi."
9 Ndipo BWANA akamwambia Mose,
10 [k]"Waambie Waisraeli: 'Wakati mmoja
wenu au wazao wenu wanapokuwa najisi
kwa sababu ya maiti au wakiwa safarini,
hata hivyo wanaweza kuadhimisha Pasaka
ya BWANA. 11 [l]Wataiadhimisha wakati wa
kuzama jua siku ya kumi na nne ya mwezi
wa pili. Watamla mwana-kondoo, pamoja na
mkate usiotiwa chachu, na mboga chungu.
12 [m]Wasibakize chochote hadi asubuhi wala
wasivunje mifupa ya mwana-kondoo.
Wakati wanapoadhimisha Pasaka, hawana
budi kufuata masharti yote. 13 [n]Lakini kama
mtu ni safi kwa taratibu za kiibada naye
hayuko safarini, asipoadhimisha Pasaka,
mtu huyo hana budi kukatiliwa mbali na
watu wake kwa sababu hakutoa sadaka ya
BWANA kwa wakati ulioamriwa. Mtu huyo
atawajibika kubeba matokeo ya dhambi
yake.
14 [o]" 'Mgeni anayeishi miongoni mwenu
ambaye anataka kuadhimisha Pasaka ya
BWANA, lazima afanye hivyo kwa kufuata
desturi na masharti. Lazima masharti yawe
sawasawa kwa mgeni na mzawa.' "

*Wingu La Moto Juu Ya Maskani*

**(Kutoka 40:34-38)**

15 [p]Katika siku hiyo ambayo Maskani,
Hema la Ushuhuda, iliposimamishwa, wingu

[a]**8:22** 2Nya 30:15
[b]**8:24** 1Nya 23:3; Kut 38:21; Hes 4:3
[c]**8:25** 1Nya 23:28-31; Eze 44:8-11
[d]**9:1** Hes 1:1; Kut 40:2
[e]**9:2** Kut 12:11; Hes 28:16; Ebr 10:1
[f]**9:3** Kut 12:2-11, 43-49; Law 23:5-8; Kum 16:1-8
[g]**9:4** Kut 12:11
[h]**9:5** Kut 12:6; Yos 5:10
[i]**9:6** Law 5:3; 13:3; 21:11; Kut 18:15; Hes 27:2; Yn 18:28; Hes 6:6-7
[j]**9:8** Kut 18:15; Law 24:12; Hes 15:34; 27:5, 21; Za 85:8; Yn 7:17; Efe 1:9, 18; Ebr 3:5-6
[k]**9:10** 2Nya 30:2
[l]**9:11** Kut 12:6-8; 2Nya 30:2, 15
[m]**9:12** Kut 12:8, 10, 43, 46; Yn 19:36
[n]**9:13** Mwa 17:14; Kut 12:15; Law 17:4; Ebr 12:25; Hes 5:31; Gal 3:10; Ebr 10:26
[o]**9:14** Kut 12:19, 43-49
[p]**9:15** Kut 38:21; 26:30; 33:16; 13:21; 40:34

liliifunika. Kuanzia jioni mpaka asubuhi
wingu lililokuwa juu ya Maskani lilionekana
kama moto. 16 [a]Hivyo ndivyo lilivyoendelea
kuwa; wingu liliifunika wakati wa mchana,
na usiku lilionekana kama moto. 17 [b]Wakati
wowote wingu lilipoinuka kutoka juu ya
Hema, nao Waisraeli waliondoka; mahali
popote wingu liliposimama, Waisraeli
walipiga kambi. 18 [c]Kwa amri ya Bwana
Waisraeli waliondoka, na kwa amri yake
walipiga kambi. Kwa muda wote wingu
liliposimama juu ya Maskani, Waisraeli
walibaki wamepiga kambi.

19 [d]Wakati wingu lilipobaki juu ya Maskani
kwa muda mrefu, Waisraeli walitii amri
ya Bwana nao hawakuondoka. 20 [e]Wakati
mwingine wingu lilikuwa juu ya Maskani
kwa siku chache tu; kwa amri ya Bwana
wangelipiga kambi na kisha kwa amri yake
wangeliondoka. 21 [f]Wakati mwingine wingu
lilikuwepo kuanzia jioni mpaka asubuhi tu,
na lilipoinuka asubuhi, nao waliondoka.
Ikiwa ni mchana au usiku, wakati wowote
wingu lilipoinuka, waliondoka. 22 Ikiwa
wingu lilikaa juu ya Maskani kwa siku mbili
au mwezi au mwaka, Waisraeli wangebaki
wamepiga kambi na hawakuondoka; lakini
lilipoinuka, wangeondoka.

23 [g]Kwa amri ya Bwana walipiga kambi,
na kwa amri ya Bwana waliondoka. Walitii
amri ya Bwana, kufuatana na agizo lake
kupitia Mose.

### *Tarumbeta Za Fedha*

10 Bwana akamwambia Mose:
2 [h]"Tengeneza tarumbeta mbili za
fedha ya kufua, uzitumie kwa kuita
jumuiya pamoja na wakati wa kuvunja
makambi ili kuondoka. 3 Tarumbeta zote
mbili zikipigwa, jumuiya yote itakusanyika
mbele yako katika ingilio la Hema la
Kukutania. 4 [i]Kama tarumbeta moja tu
ikipigwa, viongozi, yaani wakuu wa koo za
Israeli, ndio watakaokusanyika mbele yako.
5 Wakati mlio wa kujulisha hatari ukipigwa,
makabila yaliyo na makambi upande wa
mashariki yataondoka. 6 Ukisikika mlio
wa pili wa jinsi hiyo, walioko kwenye
makambi ya kusini wataondoka. Mlio
huo wa kujulisha hatari utakuwa ishara
ya kuondoka. 7 [j]Ili kukusanya kusanyiko,
piga tarumbeta zote, lakini siyo kwa mlio
wa kujulisha hatari.

8 [k]"Wana wa Aroni, makuhani, ndio
watakaopiga hizo tarumbeta. Hili litakuwa
agizo la kudumu kwa ajili yenu na kwa
vizazi vijavyo. 9 [l]Wakati mtakapopigana
vita katika nchi yenu wenyewe dhidi
ya adui anayewaonea, piga tarumbeta
kwa mlio wa kujulisha hatari. Ndipo
utakumbukwa na Bwana Mungu wenu na
kuokolewa kutoka kwa adui zenu. 10 [m]Pia
nyakati za furaha yenu, yaani sikukuu
zenu zilizoamriwa na sikukuu za Mwezi
Mwandamo, mtapiga tarumbeta juu ya
sadaka zenu za kuteketezwa na sadaka zenu
za amani, nazo zitakuwa ukumbusho kwa
ajili yenu mbele za Mungu wenu. Mimi
ndimi Bwana, Mungu wenu."

### *Waisraeli Waondoka Sinai*

11 [n]Katika siku ya ishirini ya mwezi wa pili
wa mwaka wa pili, wingu liliinuka kutoka
juu ya maskani ya Ushuhuda. 12 [o]Ndipo
Waisraeli wakaondoka kutoka Jangwa
la Sinai wakasafiri kutoka sehemu moja

---

[a]**9:16** Kut 40:38; Kum 1:33; Neh 9:12
[b]**9:17** Kut 40:36-38; 1Kor 10:1; Za 78:14; Isa 49:10; Yn 10:4; Hes 9:21; Kut 13:21, 22
[c]**9:18** Kut 40:37
[d]**9:19** Law 8:35; Kut 40:37
[e]**9:20** Za 48:14; Mit 3:5-6
[f]**9:21** Mt 28:20
[g]**9:23** Za 73:24; 107:7; Isa 63:14
[h]**10:2** Hes 31:6; Neh 4:18; 12:35; Za 47:5; 98:6; 105:3; Yer 4:5; 19; 6:1; Hos 5:8; 8:1; Yoe 2:1
[i]**10:4** Kut 18:21; Hes 7:2
[j]**10:7** Yer 4:5; 6:1; Eze 33:3; Yoe 2:1; 1Kor 14:8
[k]**10:8** Mwa 9:12; Hes 15:14; 35:29; Yos 6:4; 2Nya 13:12
[l]**10:9** Kut 3:9; Amu 2:18; 6:9; 1Sam 10:18; 2Fal 13:4; Za 106:42; Law 23:24; 2Nya 13:12; Mwa 8:1
[m]**10:10** Hes 28:11; 1Sam 20:5, 24; 2Fal 4:23; 2Nya 8:13; Za 81:3; Isa 1:13; Eze 45:17; 46:6; Amo 8:5; Law 23:24; 1:3; 3:1; 11:44; Hes 6:14
[n]**10:11** Kut 38:21; 40:17; Hes 9:17
[o]**10:12** Mwa 14:6; Kum 1:1; 33:2; Kut 40:36; Hes 12:16; Hab 3:3

hadi nyingine mpaka wingu lilipotua katika
Jangwa la Parani. 13 [a]Waliondoka kwa mara
ya kwanza kwa agizo la Bwana kupitia
kwa Mose.
14 [b]Vikosi vya kambi ya Yuda vilitangulia
kwanza chini ya alama yao. Nashoni
mwana wa Aminadabu alikuwa kiongozi
wao. 15 [c]Nethaneli mwana wa Suari alikuwa
kiongozi wa kabila la Isakari, 16 [d]naye Eliabu
mwana wa Heloni alikuwa kiongozi wa
kabila la Zabuloni. 17 [e]Ndipo Maskani
iliposhushwa, nao wana wa Gershoni
na wana wa Merari ambao waliibeba
wakaondoka.
18 [f]Vikosi vya kambi ya Reubeni
vilifuata, chini ya alama yao. Elisuri
mwana wa Shedeuri alikuwa kiongozi
wao. 19 Shelumieli mwana wa Surishadai
aliongoza kikosi cha kabila la Simeoni,
20 [g]naye Eliasafu mwana wa Deueli
aliongoza kikosi cha kabila la Gadi. 21 [h]Kisha
Wakohathi wakaondoka, wakichukua vitu
vitakatifu. Maskani ilikuwa isimamishwe
kabla wao hawajafika.
22 [i]Vikosi vya kambi ya Efraimu vilifuata,
chini ya alama yao. Elishama mwana wa
Amihudi alikuwa kiongozi wao. 23 Gamalieli
mwana wa Pedasuri aliongoza kikosi cha
kabila la Manase, 24 [j]naye Abidani mwana
wa Gideoni alikuwa kiongozi wa kikosi cha
kabila la Benyamini.
25 [k]Mwishowe, kama kikosi cha nyuma
cha ulinzi wa vikosi vyote, vikosi vya kambi
ya Dani viliondoka chini ya alama yao.
Ahiezeri mwana wa Amishadai alikuwa
kiongozi wao. 26 Pagieli mwana wa Okrani
aliongoza kikosi cha kabila la Asheri,
27 naye Ahira mwana wa Enani aliongoza
kikosi cha kabila la Naftali. 28 [l]Huu ndio
ulikuwa utaratibu wa kuondoka wa vikosi
vya Waisraeli walipokuwa wanaondoka.
29 [m]Basi Mose akamwambia Hobabu
mwana wa Reueli, Mmidiani, mkwewe
Mose, "Tunaondoka kwenda mahali
ambapo Bwana amesema 'Nitawapa
ninyi mahali hapo.' Twende pamoja nasi
tutakutendea mema, kwa maana Bwana
ameahidi mambo mema kwa Israeli."
30 [n]Akajibu, "Hapana, sitakwenda;
nitarudi kwenye nchi yangu mwenyewe
na watu wangu mwenyewe."
31 [o]Lakini Mose akasema, "Tafadhali
usituache. Wewe unajua mahali ambapo
yatupasa kupiga kambi jangwani, nawe
unaweza kuwa macho yetu. 32 [p]Ikiwa
utafuatana nasi, tutashirikiana nawe mema
yoyote tutakayopewa na Bwana."
33 [q]Hivyo waliondoka kutoka mlima wa
Bwana, nao wakasafiri kwa siku tatu.
Sanduku la Agano la Bwana liliwatangulia
kwa zile siku tatu ili kuwatafutia mahali pa
kupumzika. 34 [r]Wingu la Bwana lilikuwa
juu yao wakati wa mchana walipoondoka
kambini.
35 [s]Wakati wowote Sanduku lilipoondoka,
Mose alisema,

"Ee Bwana, inuka!
Watesi wako na watawanyike;
adui zako na wakimbie mbele
zako."

36 [t]Wakati wowote Sanduku liliposimama,
alisema,

[a]**10:13** Kum 1:6; Hes 2:34
[b]**10:14** Hes 1:52; 2:3-9; 1:7
[c]**10:15** Law 24:11; Hes 1:8
[d]**10:16** Hes 2:7; 1:9
[e]**10:17** Hes 4:21-32
[f]**10:18** Hes 2:16; 2:10-16; 1:5
[g]**10:20** Hes 1:14
[h]**10:21** Hes 2:17; 4:20
[i]**10:22** Hes 2:24; 1:10
[j]**10:24** Hes 1:11
[k]**10:25** Hes 2:31; 1:12; Yos 6:9
[l]**10:28** Za 80:1; Wim 6:10
[m]**10:29** Amu 4:11; Kut 2:18; 3:1; Mwa 12:7; 15:14
[n]**10:30** Mt 21:29; Kut 18:27
[o]**10:31** Ay 29:15
[p]**10:32** Kut 12:48; Kum 10:18; Za 22:27-31; 67:5-7
[q]**10:33** Kum 1:33; 10:8; 31:9; Yos 3:3; Amu 20:27; 2Sam 15:24; Yer 31:2
[r]**10:34** Hes 9:15-23; Kut 13:21; Neh 9:12, 19
[s]**10:35** 2Nya 6:41; Za 17:13; 44:26; 94:2; 132:8; Amu 5:31; 2Sam 2:1; Za 68:1; 92:9; Kum 5:9; 7:10; Isa 17:12-14; 59:18
[t]**10:36** Isa 52:8; 63:17; Mwa 15:5; 26:4; Kum 1:10; 10:22; Neh 9:23

"Ee BWANA, rudi,
kwa maelfu ya Waisraeli
wasiohesabika."

*Moto Kutoka Kwa BWANA*

11 [a]Basi watu wakalalamika kwa habari
ya taabu zao masikioni mwa BWANA,
naye alipowasikia, hasira yake ikawaka.
Ndipo moto kutoka kwa BWANA ukawaka
miongoni mwao na kuteketeza baadhi ya
viunga vya kambi. 2 [b]Watu walipomlilia
Mose, akamwomba BWANA, nao moto
ukazimika. 3 [c]Hivyo mahali pale pakaitwa
Tabera,[d] kwa sababu moto kutoka kwa
BWANA uliwaka miongoni mwao.

*Kware Kutoka Kwa BWANA*

4 [e]Umati wa watu wenye zogo waliokuwa
miongoni mwao walitamani sana chakula
kingine, Waisraeli wakaanza kulia tena na
kusema, "Laiti tungekuwa na nyama tule!
5 [f]Tunakumbuka wale samaki tuliokula
huko Misri bila gharama, pia yale matango,
matikitimaji, mboga, vitunguu, na vitunguu
saumu. 6 [g]Lakini sasa tumepoteza hamu
ya chakula; hatuoni kitu kingine chochote
isipokuwa hii mana!"
7 [h]Mana ilifanana kama mbegu za
giligilani, nayo ilikuwa na rangi ya manjano
iliyopauka. 8 [i]Hao watu walikwenda
kukusanya, kisha waliisaga kwa mawe ya
kusagia ya mkono au kuitwanga kwenye
vinu. Waliipika vyunguni au kutengeneza
maandazi. Ladha yake ilikuwa kama kitu
kilichotengenezwa kwa mafuta ya zeituni.
9 [j]Umande ulipoanguka kambini wakati wa
usiku, pia mana ilianguka pamoja nao.
10 Mose akasikia watu wa kila jamaa
wakilia, kila mmoja kwenye mlango wa
hema lake. BWANA akakasirika mno,
naye Mose akafadhaika. 11 [k]Akamuuliza
BWANA, "Kwa nini umeleta taabu hii juu
ya mtumishi wako? Nimekufanyia nini cha
kukuchukiza hata ukaweka mzigo huu wa
watu hawa wote juu yangu? 12 [l]Je, watu
hawa wote mimi ndiye niliyewatungisha
mimba? Je, ni mimi niliyewazaa? Kwa
nini unaniambia niwachukue mikononi
mwangu, kama vile mlezi abebavyo mtoto
mchanga, hadi kwenye nchi uliyowaahidi
baba zao? 13 [m]Nitapata wapi nyama kwa
ajili ya watu wote hawa? Wanaendelea
kunililia wakisema, 'Tupe nyama tule!'
14 [n]Mimi siwezi kuwabeba watu hawa wote
peke yangu, mzigo ni mzito sana kwangu.
15 [o]Kama hivi ndivyo unavyonitendea,
uniue sasa hivi, yaani kama nimepata
kibali machoni pako, wala usiniache nione
maangamizi yangu mwenyewe."
16 [p]BWANA akamwambia Mose: "Niletee
wazee sabini wa Israeli, unaowafahamu
kama viongozi na maafisa miongoni mwa
watu. Walete katika Hema la Kukutania,
ili waweze kusimama huko pamoja nawe.
17 [q]Nami nitashuka na kusema nawe huko.
Nami nitachukua sehemu ya Roho iliyo juu
yako na kuiweka juu yao. Watakusaidia
kubeba mzigo wa watu hao ili usije
ukaubeba peke yako.

[a]**11:1** Law 10:2; Kut 4:14; 14:11; 16:7; Mao 3:39; Hes 12:2; 21:28; Kum 1:34; Za 78:63; Isa 26:11; Kut 15:23, 24; 16:2, 3, 7; Kum 9:22; 2Fal 1:12
[b]**11:2** Kum 9:19; 1Sam 2:25; 12:23; Za 106:23; Mwa 20:7; Hes 21:7; Yn 2:1
[c]**11:3** Kum 9:20-22; Hes 16:35; Ay 1:16; Isa 10:17
[d]3 Tabera maana yake Kunaungua.
[e]**11:4** Kut 12:38; 16:3; Za 78:18; 1Kor 10:6
[f]**11:5** Kut 16:3; Hes 21:5; Flp 3:19; Mt 6:24-34; Rum 8:7
[g]**11:6** Kut 16:14
[h]**11:7** Kut 16:31; Mwa 2:12; 2:12
[i]**11:8** Kut 16:16
[j]**11:9** Kut 16:13
[k]**11:11** Mwa 34:30; Kut 5:22; 18:18; 17:4; Kum 1:12; Yer 15:10, 18; 20:7-18; Mal 3:14; 2Kor 11:28
[l]**11:12** Isa 40:11; 49:23; 66:11, 12; Hes 14:16; Mwa 12:7; Kut 13:5; Eze 34:23; Yn 10:11; 1The 2:7; Mwa 22:16; 26:3
[m]**11:13** Kut 12:37; Yn 6:5-9; 2Fal 4:43; Mt 15:33; Mk 8:4
[n]**11:14** Kut 18:18
[o]**11:15** Kut 32:32; 1Fal 19:4; Ay 6:9; 7:15-16; 9:21; Isa 38:12; Yn 4:3
[p]**11:16** Kut 3:16; 18:25; 40:2; 24:1, 9
[q]**11:17** Kut 18:18; 19:20; 1Sam 10:6; 2Fal 2:9, 15; 3:12; Isa 32:15; Yoe 2:28; Hag 2:5; Yer 19:1

18 [a]“Waambie hao watu: ‘Jiwekeni wakfu
wenyewe kwa ajili ya kesho, wakati
mtakapokula nyama. Bwana aliwasikia
mlipolia, mkisema, “Laiti tungekuwa na
nyama tule! Tulikuwa na hali nzuri zaidi
katika nchi ya Misri!” Sasa Bwana atawapa
nyama, nanyi mtaila. 19 Hamtaila kwa siku
moja tu, au siku mbili, au tano, kumi au
siku ishirini, 20 [b]bali kwa mwezi mzima
mpaka iwatokee puani, nanyi mtaichukia
kabisa, kwa kuwa mmemkataa Bwana,
ambaye yupo miongoni mwenu, nanyi
mmelia mbele zake, mkisema, “Hivi kwa
nini tulitoka Misri?” ’ ”

21 [c]Lakini Mose alisema, “Mimi niko hapa
miongoni mwa watu 600,000 wanaotembea
kwa miguu, nawe umesema, ‘Nitawapa
nyama ya kula kwa mwezi mzima!’ 22 [d]Je,
wangeweza kupata nyama ya kuwatosha
hata kama makundi ya kondoo na ya
ng’ombe yangechinjwa kwa ajili yao? Je,
wangetosheka hata kama samaki wote wa
baharini wangevuliwa kwa ajili yao?”

23 [e]Bwana akamjibu Mose, “Je, mkono
wa Bwana ni mfupi sana? Sasa utaona
kama jambo nililolisema litatimizwa kwa
ajili yako au la.”

24 Kwa hiyo Mose akatoka na kuwaambia
watu lile ambalo Bwana alikuwa
amesema. Akawakusanya wazee wao
sabini, akawasimamisha kuzunguka Hema.
25 [f]Kisha Bwana akashuka katika wingu
na kunena na Mose, naye akachukua
sehemu ya Roho iliyokuwa juu ya Mose
na kuiweka juu ya wale wazee sabini. Roho
aliposhuka juu yao, wakatoa unabii, lakini
hawakufanya hivyo tena.

26 [g]Lakini, watu wawili, ambao majina
yao ni Eldadi na Medadi, walibaki kambini.
Walikuwa wameorodheshwa miongoni
mwa wale wazee sabini, lakini hawakutoka
kwenda kwenye Hema. Lakini Roho pia
alishuka juu yao, nao wakatabiri huko
kambini. 27 Mwanaume mmoja kijana
alikimbia na kumwambia Mose, “Eldadi
na Medadi wanatoa unabii kambini.”

28 [h]Yoshua mwana wa Nuni, ambaye
alikuwa msaidizi wa Mose tangu ujana
wake, akajibu akasema, “Mose bwana
wangu, wanyamazishe!”

29 [i]Lakini Mose akajibu, “Je, unaona
wivu kwa ajili yangu? Ningetamani watu
wote wa Bwana wangekuwa manabii na
kwamba Bwana angeweka Roho yake juu
yao!” 30 Ndipo Mose na wale wazee wa
Israeli wakarudi kambini.

31 [j]Kisha ukatokea upepo kutoka kwa
Bwana, nao ukawaletea kware kutoka
baharini. Ukawaangusha kwenye eneo lote
linalozunguka kambi na kujaa ardhini kimo
cha mita moja hivi kutoka ardhini kwenye
eneo la umbali wa mwendo wa siku moja
kila upande. 32 [k]Mchana kutwa na usiku
kucha pamoja na siku nzima iliyofuata watu
walitoka kwenda kuokota kware. Hakuna
mtu yeyote aliyekusanya chini ya homeri
kumi.[l] Kisha wakazianika kuzunguka kambi
yote. 33 [m]Lakini walipokuwa wakila nyama,
ilipokuwa ingali kati ya meno yao na kabla
hawajamaliza kula, hasira ya Bwana
ikawaka dhidi ya watu, naye akawapiga
kwa tauni. 34 [n]Kwa hiyo mahali hapo
pakaitwa Kibroth-Hataava,[o] kwa sababu
huko ndiko walipowazika watu ambao
walitamani sana chakula kingine.

---

[a]**11:18** Kut 19:10; 16:7; Mdo 7:39; Za 78:20
[b]**11:20** Za 78:29; 106:14-15; Law 26:43; Ay 1:14; 20:13, 23; Yos 24:27; Amu 8:23; 1Sam 10:19; Isa 59:13; Hos 13:11
[c]**11:21** Kut 12:37
[d]**11:22** Mt 15:33; 2Fal 7:2; Mk 6:37
[e]**11:23** Isa 50:2; 59:1; Hes 23:19; 1Sam 15:29; Eze 12:25; 24:14
[f]**11:25** Kut 19:9; Hes 12:5; 1Sam 10:6, 10; 19:20, 23; Mdo 2:17; Amu 3:10; Kut 34:5; 40:38; 2Fal 2:15; Yoe 2:29; 1Kor 14:1
[g]**11:26** 1Nya 12:18; Ufu 1:10; 1Sam 20:26; Yer 36:5
[h]**11:28** Kut 17:9; 33:11; Hes 13:8; 26:65; Yos 14:10; Mk 9:38-40; Mdo 26:29; 1Kor 14:5
[i]**11:29** 1Sam 10:5; 19:20; 2Nya 24:19; Yer 7:25; 44:4; 1Kor 14:5; Hes 27:18
[j]**11:31** Kut 16:13; Za 78:26-28
[k]**11:32** Kut 16:36; Eze 45:11
[l]32 Homeri 10 ni sawa na kilo 1,000.
[m]**11:33** Za 78:30; 106:15, 29; Hes 14:18; Kum 9:7; Amu 2:12; 2Fal 22:17; Yer 44:3; Eze 8:17; Isa 10:16
[n]**11:34** Hes 33:16; Kum 9:22
[o]34 Kibroth-Hataava maana yake Makaburi ya wenye tamaa nyingi.

35 [a]Kutoka Kibroth-Hataava watu wakasafiri mpaka Haserothi na kukaa huko.

*Miriamu Na Aroni Wampinga Mose*

12 [b]Miriamu na Aroni walianza kuzungumza dhidi ya Mose kwa sababu ya mke wake Mkushi, kwa kuwa
alikuwa ameoa Mkushi. 2 [c]Waliuliza, "Je,
BWANA amesema kupitia Mose peke yake? Je, hajasema kutupitia sisi pia?" Naye BWANA akasikia hili.

3 [d](Basi Mose alikuwa mtu mnyenyekevu sana, mnyenyekevu kuliko mtu mwingine yeyote katika uso wa dunia.)

4 Ghafula BWANA akawaambia Mose, Aroni na Miriamu, "Njooni katika Hema la Kukutania, ninyi nyote watatu." Kwa
hiyo wote watatu wakaenda. 5 [e]Kisha
BWANA akashuka katika nguzo ya wingu, akasimama kwenye ingilio la Hema, akawaita Aroni na Miriamu. Wakati wote
wawili waliposogea mbele, 6 [f]BWANA
akasema, "Sikilizeni maneno yangu:

"Akiwapo nabii wa BWANA
miongoni mwenu,
nitajifunua kwake kwa maono,
nitanena naye katika ndoto.
7 [g]Lakini sivyo kwa mtumishi wangu
Mose;
yeye ni mwaminifu katika nyumba
yangu yote.
8 [h]Kwake nitanena naye uso kwa uso,
waziwazi wala si kwa mafumbo;
yeye ataona umbo la BWANA.
Kwa nini basi ninyi hamkuogopa
kuzungumza kinyume cha
mtumishi wangu Mose?"

9 [i]Hasira ya BWANA ikawaka dhidi yao, akawaacha.

10 [j]Wakati hilo wingu liliinuka kutoka juu ya Hema, Miriamu akawa tayari ana ukoma, mweupe kama theluji. Aroni
akamgeukia, akaona ana ukoma. 11 [k]Kisha
Aroni akamwambia Mose, "Tafadhali, bwana wangu, usituhesabie dhambi hii ambayo tumeifanya kwa upumbavu.
12 [l]Usimwache awe kama mtoto mchanga aliyezaliwa akiwa mfu, ambaye nusu ya mwili wake imeharibika hapo atokapo katika tumbo la mama yake."

13 [m]Hivyo Mose akamlilia BWANA akisema, "Ee Mungu, nakuomba umponye!"

14 [n]BWANA akamjibu Mose, "Je, kama baba yake angemtemea usoni, asingeona aibu kwa siku saba? Mfungie nje ya kambi kwa siku saba; baada ya hapo anaweza
kurudishwa kambini." 15 [o]Kwa hiyo Miriamu
akafungiwa nje ya kambi kwa siku saba, nao watu hawakuendelea na safari mpaka aliporudishwa kambini.

16 [p]Baada ya hayo, watu waliondoka Haserothi, wakapiga kambi katika Jangwa la Parani.

*Kupeleleza Kanaani*

**(Kumbukumbu 1:19-33)**

13 BWANA akamwambia Mose, 2 [q]"Watume
baadhi ya watu wakaipeleleze nchi ya Kanaani, ambayo ninawapa Waisraeli.

---

[a]**11:35** Hes 33:17; Kum 1:1
[b]**12:1** Kut 15:20; 2:21
[c]**12:2** Hes 16:3; 11:1; Mwa 29:33; Mik 6:4; 2Fal 19:4; Za 94:9; Eze 35:12
[d]**12:3** Mt 11:29; 1Tim 6:11; 2Tim 2:25; Za 149:4; 1Pet 3:4
[e]**12:5** Kut 13:21; Hes 11:25; Kut 34:5
[f]**12:6** 1Sam 3:7, 21; Mwa 15:1; 20:3; 46:2; Mt 27:19; Ebr 1:1; 1Fal 3:5; Mwa 46:2; Ay 33:15; Lk 1:11; 1:22; Mt 1:20
[g]**12:7** Kum 34:5; Yos 1:1-2; Za 105:26; Ebr 3:2, 5
[h]**12:8** Amu 14:12; 1Fal 10:1; Za 17:15; 49:4; 140:13; Mit 1:6; Dan 5:12; Kut 20:4; 24:2; Ay 19:26; Isa 6:1
[i]**12:9** Kut 4:14; Mwa 17:22
[j]**12:10** Kut 4:6; 40:2; Kum 24:9; Law 13:11; 2Fal 5:1, 27; 2Nya 16:12; 21:12
[k]**12:11** 2Sam 19:19; 24:10
[l]**12:12** Za 88:4; Efe 2:1-5; Kol 2:13; 1Tim 5:6
[m]**12:13** Kut 15:26; Za 6:2; 147:3; Isa 1:6; 30:26; 53:5; Yer 17:14; Hos 6:1
[n]**12:14** Kum 25:9; Ay 17:6; 30:9-10; Isa 50:6; Law 13:46; Hes 5:2-3; Ebr 12:9; 2Nya 26:20, 21
[o]**12:15** Law 14:8; 13; Kum 24:9
[p]**12:16** Hes 10:12; 11:35; 15:32; Mwa 21:21
[q]**13:2** Hes 13:16; Kum 1:22; Law 14:34; 24:11; Yos 1:3

Kutoka kwa kila kabila la baba zao, tuma
mmoja wa viongozi wao.”
3 [a]Hivyo kwa agizo la BWANA Mose
akawatuma kutoka Jangwa la Parani. Wote
walikuwa viongozi wa Waisraeli. 4 Haya
ndiyo majina yao:

kutoka kabila la Reubeni, Shamua mwana wa Zakuri;
5 kutoka kabila la Simeoni, Shafati mwana wa Hori;
6 [b]kutoka kabila la Yuda, Kalebu mwana wa Yefune;
7 kutoka kabila la Isakari, Igali mwana wa Yosefu;
8 [c]kutoka kabila la Efraimu, Hoshea mwana wa Nuni;
9 kutoka kabila la Benyamini, Palti mwana wa Rafu;
10 kutoka kabila la Zabuloni, Gadieli mwana wa Sodi,
11 kutoka kabila la Manase (kabila la Yosefu), Gadi mwana wa Susi;
12 kutoka kabila la Dani, Amieli mwana wa Gemali;
13 kutoka kabila la Asheri, Sethuri mwana wa Mikaeli;
14 kutoka kabila la Naftali, Nabi mwana wa Wofsi;
15 kutoka kabila la Gadi, Geueli mwana wa Maki.

16 [d]Haya ndiyo majina ya watu ambao Mose
aliwatuma kuipeleleza nchi. (Mose akampa
Hoshea mwana wa Nuni jina Yoshua.)
17 [e]Mose alipowatuma wakaipeleleze
Kanaani, alisema, “Pandeni kupitia
Negebu, mwende mpaka nchi ya vilima.
18 Mwone nchi ni ya namna gani, na kama
watu waishio humo wana nguvu au ni
wadhaifu, iwapo ni wachache au wengi.
19 Wanaishi katika nchi ya namna gani? Je,
ni nzuri au mbaya? Wanaishi katika miji
ya namna gani? Je, haina kuta au ngome?
20 [f]Ardhi iko aje? Ina rutuba au la? Je, kuna
miti ndani yake au la? Jitahidini kadiri
mwezavyo kuleta baadhi ya matunda ya
nchi.” (Ulikuwa msimu wa kuiva zabibu
za kwanza.)
21 [g]Hivyo wakapanda na kuipeleleza
nchi kutoka Jangwa la Sini hadi Rehobu,
kuelekea Lebo-Hamathi. 22 [h]Wakapanda
kupitia Negebu hadi wakafika Hebroni,
mahali ambapo Ahimani, Sheshai na
Talmai, wazao wa Anaki, waliishi. (Hebroni
ulikuwa umejengwa miaka saba kabla ya
mji wa Soani ulioko Misri.) 23 [i]Walipofika
katika Bonde la Eshkoli, walivunja tawi
lililokuwa na kishada kimoja cha zabibu.
Wawili wao wakalichukua lile tawi kwenye
mti, pamoja na komamanga na tini. 24 Eneo
lile likaitwa Bonde la Eshkoli kwa sababu ya
kile kishada cha zabibu ambacho Waisraeli
walikikata huko. 25 [j]Mwishoni mwa siku
arobaini wakarudi kutoka kuipeleleza nchi.

*Taarifa Juu Ya Upelelezi*

26 [k]Wakarudi kwa Mose, Aroni na jumuiya
yote ya Waisraeli huko Kadeshi kwenye
Jangwa la Parani. Hapo ndipo walipotoa
habari kwao na kwa kusanyiko lote na
kuwaonyesha matunda ya hiyo nchi.
27 [l]Wakampa Mose taarifa hii: “Tuliingia
katika nchi uliyotutuma, nayo inatiririka
maziwa na asali! Hili hapa tunda lake.
28 [m]Lakini watu wanaoishi huko ni wenye
nguvu, na miji yao ina ngome na ni mikubwa

[a]**13:3** Hes 14:6; 24; 34:19; Kum 1:36; Amu 1:12-15
[b]**13:6** Hes 14:6; 24; 34:19; Kum 1:36; Amu 1:12-15; Yos 14:6
[c]**13:8** Hes 11:28
[d]**13:16** Kum 32:44; Kut 17:9
[e]**13:17** Yos 14:7; Mwa 12:9; Kum 1:7; Yos 9:1; Mwa 14:10; Kum 1:19; Amu 1:9-10
[f]**13:20** Kum 1:25; Law 25:5; Kum 8:7, 8; Neh 9:25-35; Eze 20:6; 34:14; Kum 31:6; Yos 1:6, 9; Ebr 13:6
[g]**13:21** Hes 20:1; 27:14; 33:36; 34:8; Kum 32:51; Yos 15:1; 19:28; 13:5; Amu 1:31; 18:28; 2Sam 10:6; 1Nya 6:75; 13:5; 1Fal 8:65; 2Fal 14:25; 2Nya 7:8; Yer 52:7; Eze 47:16-20; Amo 6:14
[h]**13:22** Hes 13:28; Mwa 13:18; 23:19; Yos 15:14; Amu 1:10; Kum 2:10; 9:2; Yos 11:21; 15:13; Za 78:12; Isa 19:11-13; 30:4; Eze 30:14
[i]**13:23** Mwa 14:13; Kut 28:33; Mwa 3:7; Hes 20:5; Kum 8:8; 2Fal 18:31; Neh 13:15
[j]**13:25** Mwa 7:4; Hes 14:34
[k]**13:26** Mwa 14:6-7; Hes 32:8; Kum 1:25
[l]**13:27** Kut 3:8; Kum 1:25; Yer 2:7
[m]**13:28** Kum 1:28; Yos 14:12

sana. Huko tuliona hata wazao wa Anaki.
29 [a]Waamaleki wanaishi Negebu; Wahiti,
Wayebusi na Waamori wanaishi katika nchi
ya vilima; nao Wakanaani wanaishi karibu
na bahari na kando ya Yordani."
30 [b]Kisha Kalebu akawanyamazisha watu
mbele ya Mose na kusema, "Imetupasa
kupanda na kuimiliki nchi, kwa maana
hakika tunaweza kufanya hivyo."
31 [c]Lakini watu waliokuwa wamepanda
pamoja naye wakasema, "Hatuwezi
kuwashambulia wale watu; wana nguvu
kutuliko sisi." 32 [d]Wakaeneza taarifa
mbaya miongoni mwa Waisraeli kuhusu
nchi waliyoipeleleza. Wakasema, "Nchi
tuliyoipeleleza hula watu waishio ndani
yake. Watu wote tuliowaona huko ni majitu.
33 [e]Tuliwaona Wanefili huko (wazao wa
Anaki wanatokana na Wanefili.) Tulijiona
kama panzi machoni petu wenyewe, nao
ndivyo walivyotuona."

*Watu Wanaasi*

14 [f]Usiku ule watu wote wa jumuiya
walipaza sauti zao na kulia kwa sauti
kuu. 2 [g]Waisraeli wote wakanung'unika
dhidi ya Mose na Aroni, nalo kusanyiko lote
wakawaambia, "Laiti tungekuwa tumefia
humo nchi ya Misri! Au humu kwenye
hili jangwa! 3 [h]Kwa nini BWANA anatuleta
katika nchi hii ili tufe kwa upanga? Wake
zetu na watoto wetu watachukuliwa kama
nyara. Je, isingekuwa bora kwetu kurudi
Misri?" 4 [i]Wakasemezana wao kwa wao,
"Inatupasa kumchagua kiongozi na kurudi
Misri."
5 [j]Ndipo Mose na Aroni wakaanguka
kifudifudi mbele ya kusanyiko lote la
Kiisraeli lililokusanyika hapo. 6 [k]Yoshua
mwana wa Nuni na Kalebu mwana wa
Yefune, waliokuwa miongoni mwa watu wale
waliokwenda kuipeleleza nchi, wakararua
nguo zao, 7 [l]wakasema na kusanyiko lote
la Kiisraeli, wakawaambia, "Nchi tuliyopita
katikati yake na kuipeleleza ni nzuri sana
sana. 8 [m]Ikiwa BWANA anapendezwa nasi,
atatuongoza kuingia katika nchi ile, nchi
itiririkayo maziwa na asali, naye atatupa
nchi hiyo. 9 [n]Ila tu msimwasi BWANA. Wala
msiwaogope watu wa nchi hiyo, kwa sababu
tutawameza. Ulinzi wao umeondoka, lakini
BWANA yupo pamoja nasi. Msiwaogope."
10 [o]Lakini kusanyiko lote likazungumza
juu ya kuwapiga kwa mawe. Ndipo
utukufu wa BWANA ukaonekana katika
Hema la Kukutania kwa Waisraeli wote.
11 [p]BWANA akamwambia Mose, "Watu hawa
watanidharau mpaka lini? Wataendelea
kukataa kuniamini mimi mpaka lini,
ingawa nimetenda ishara za miujiza
miongoni mwao? 12 [q]Nitawapiga kwa tauni
na kuwaangamiza, lakini nitakufanya wewe
kuwa taifa kubwa lenye nguvu kuliko wao."
13 [r]Mose akamwambia BWANA, "Ndipo

---

[a]**13:29** Mwa 10:16, 18; 13:10; 14:7; 10:15; Kum 7:1; 20:17; 1Fal 9:20; 10:29; 2Fal 6:7; Kut 3:8; Hes 22:1; 32:5; Amu 3:28; Za 42:6
[b]**13:30** Yos 14:7; Za 60:12; 119:10; Isa 11:10; Rum 8:31; Flp 4:13; Ebr 11:33, 34
[c]**13:31** Kum 9:1; Yos 14:8
[d]**13:32** Hes 14:36-37; Eze 36:13-14; Kum 1:28; Amo 2:9
[e]**13:33** Mwa 6:4; Kum 1:28; Yos 11:22; 14:12; Mhu 12:5; Isa 40:22
[f]**14:1** Mwa 27:38; Kut 33:4; Hes 25:6; Kum 1:45; Amu 20:23-26; 2Sam 3:32; Ay 31:29
[g]**14:2** Kut 16:3; 15:24; Ebr 3:16; Hes 11:1; 16:13; 20:4; 21:5
[h]**14:3** Kut 5:21; Kum 1:39; Mwa 34:29; Za 109:11; Isa 33:4; Eze 7:21; 25:7; 26:5; Mdo 7:39
[i]**14:4** Neh 9:17; Mdo 7:36; Ebr 11:15
[j]**14:5** Law 9:24; 19:2; Hes 16:4, 22, 45; 20:6; Yos 5:12; Eze 1:28; 2Sam 14:4; 1Nya 21:16
[k]**14:6** Hes 11:28; Mwa 37:29-34; Amu 11:35; 2Sam 13:31; 1Fal 19:1; Ezr 9:3; Es 4:1; Mk 14:63
[l]**14:7** Hes 13:27; Kum 1:25
[m]**14:8** Kum 1:21; 7:8; 10:15; Za 18:19; 22:8; 37:23; 41:11; 56:9; 147:11; Mit 11:20; Isa 62:4; Mal 2:17; Hes 13:27
[n]**14:9** Kum 1:21, 26; 7:18; 9:7; 20:1; Mwa 21:22; 26:24; 2Nya 13:12; 32:7; Za 118:6; Hag 2:4; 1:13; Yer 15:20; 41:18; 42:11; 46:28
[o]**14:10** Kut 17:4; 24:16; Law 9:24
[p]**14:11** Kut 3:20; 4:17; 10:1; 23:21; Hes 15:31; 16:30; 1Sam 2:17; Yn 3:25; Eze 31:14; Mal 1:13; Kum 1:32; Za 78:22; 106:24
[q]**14:12** Kut 5:3; 33:10; Kum 9:14; 29:20; 32:26; Za 109:13
[r]**14:13** Kut 32:11; Za 106:23

Wamisri watasikia juu ya jambo hili!
Kwa uweza wako uliwapandisha watu
hawa kutoka miongoni mwao. 14 [a]Nao
watawaambia wenyeji wa nchi hii jambo
hili. Wao tayari wameshasikia kwamba
wewe, Ee BWANA, upo pamoja na watu
hawa, na kuwa wewe, Ee BWANA,
umeonekana uso kwa uso, nalo wingu lako
hukaa juu yao. Tena wewe unawatangulia
kwa nguzo ya wingu mchana na kwa nguzo
ya moto usiku. 15 Ikiwa utawaua watu hawa
wote mara moja, mataifa ambayo yamesikia
taarifa hii kukuhusu wewe watasema,
16 [b]‘BWANA alishindwa kuwaingiza watu
hawa katika nchi aliyowaahidi kwa kiapo;
hivyo akawaua jangwani.’

17 “Basi sasa nguvu za Bwana na
zionekane, sawasawa na vile ulivyosema:
18 [c]‘BWANA si mwepesi wa hasira, ni
mwingi wa upendo na mwenye kusamehe
dhambi na uasi. Lakini haachi kumwadhibu
mwenye hatia, huadhibu watoto kwa ajili
ya dhambi ya baba zao hata kizazi cha tatu
na cha nne.’ 19 [d]Kwa kadiri ya upendo wako
mkuu, usamehe dhambi ya watu hawa,
kama vile ulivyowasamehe tangu wakati
walitoka Misri mpaka sasa.”

20 [e]BWANA akajibu, “Nimewasamehe
kama ulivyoomba. 21 [f]Hata hivyo, kwa
hakika kama niishivyo, na kwa hakika
kama utukufu wa BWANA uijazavyo dunia
yote, 22 [g]hakuna hata mmoja wa watu hawa
ambao waliuona utukufu wangu na ishara
za miujiza niliyotenda huko Misri na huko
jangwani, lakini ambaye hakunitii na
akanijaribu mara hizi kumi, 23 [h]hakuna hata
mmoja wao atakayeona nchi niliyowaahidi
baba zao kwa kiapo. Hakuna hata mmoja
ambaye amenidharau atakayeiona.
24 [i]Lakini kwa sababu mtumishi wangu
Kalebu ana roho ya tofauti na ananifuata
kwa moyo wote, nitamwingiza katika nchi
aliyoiendea, nao wazao wake watairithi.
25 [j]Kwa kuwa Waamaleki na Wakanaani
wanaishi katika mabonde, kesho geukeni
mwelekee jangwani kwa kufuata njia
iendayo Bahari ya Shamu.”[k]

26 [l]BWANA akamwambia Mose na Aroni:
27 [m]“Jumuiya hii ovu itanung’unika dhidi
yangu hadi lini? Nimesikia malalamiko
ya hawa Waisraeli wanaonung’unika.
28 [n]Hivyo waambie, ‘Hakika kama niishivyo,
asema BWANA, nitawafanyia vitu vilevile
nilivyosikia mkisema: 29 [o]Kila mmoja wenu
mwenye umri wa miaka ishirini au zaidi
ambaye alihesabiwa na amenung’unika
dhidi yangu, miili yenu itaanguka katika
jangwa hili. 30 [p]Hakuna hata mmoja wenu
atakayeingia katika nchi niliyoapa kwa
mkono ulioinuliwa kuwa makao yenu,
isipokuwa Kalebu mwana wa Yefune, na
Yoshua mwana wa Nuni. 31 [q]Lakini watoto
wenu ambao mlisema watachukuliwa kama
mateka, nitawaingiza humo ili waifurahie
nchi ambayo ninyi mmeikataa. 32 [r]Lakini
ninyi, miili yenu itaanguka katika jangwa
hili. 33 [s]Watoto wenu watakuwa wachungaji

---

[a]**14:14** Kut 13:21; 15:14; 33:16; Hes 5:3; 16:3; Yos 2:9; Kum 5:4; 34:10
[b]**14:16** Hes 11:12; Kut 32:12; Yos 7:7
[c]**14:18** Kut 20:5-6; 34:6; Za 145:8; Yon 4:2; Yak 5:11
[d]**14:19** Kut 34:9; 1Fal 8:34; Za 85:2; 103:3; 10:6; 65; 78:38
[e]**14:20** Kut 34:6; Za 99:8; 106:23; Mik 7:18-20
[f]**14:21** Hes 14:28; Kum 32:40; Amu 8:19; Rut 3:13; 1Sam 14:39; 19:6; Isa 6:3; 40:5; 49:18; Yer 4:2; Eze 5:11; Law 9:6; Za 72:19; Hab 2:14
[g]**14:22** Kut 14:11; 17:7; 32:1; Za 81:7; 1Kor 10:5
[h]**14:23** Kut 33:1; Hes 32:11; Kum 1:34; Ebr 3:18; Za 95:11; 106:26
[i]**14:24** Hes 13:6; 26:65; 32:12; Kum 1:36; Yos 14:8, 14; Za 25:13; 37:9-11
[j]**14:25** Mwa 14:7; 10:18; Kum 1:40; Kut 23:31; Hes 21:4; 1Fal 9:26
[k]25 Yaani Bahari Nyekundu au Bahari ya Mafunjo.
[l]**14:26** Kut 16:12; Kum 1:34-35
[m]**14:27** Kut 16:28; Mt 17:17; Mk 9:19; Kut 16:12; 1Kor 10:10
[n]**14:28** Hes 33:56; Ebr 3:17
[o]**14:29** Hes 1:45; 26:65; 32:13; 1Kor 10:5; Ebr 3:17; Yud 5; Kut 30:12
[p]**14:30** Kut 6:8; Kum 32:40; Neh 9:15; Za 106:26; Eze 20:5; 36:7; Hes 13:6; 11:28
[q]**14:31** Law 26:43
[r]**14:32** 1Kor 10:5
[s]**14:33** Kut 16:35; Mdo 13:18; Ebr 3:9

wa mifugo hapa kwa miaka arobaini,
wakiteseka kwa ajili ya kukosa uaminifu
kwenu, hadi mwili wa mtu wenu wa
mwisho ulale katika jangwa hili. 34 [a]Kwa
miaka arobaini, mwaka mmoja kwa kila
siku katika zile siku arobaini mlizoipeleleza
nchi, mtateseka kwa ajili ya dhambi zenu,
na kujua jinsi ilivyo vibaya kunifanya
mimi kuwa adui yenu.' 35 [b]Mimi BWANA
nimesema, na hakika nitafanya mambo
haya kwa jumuiya hii yote ovu, ambayo
imefungamana pamoja dhidi yangu.
Watakutana na mwisho wao katika jangwa
hili; hapa ndipo watafia."
36 [c]Hivyo watu wale ambao Mose
alikuwa amewatuma kuipeleleza nchi,
waliorudi na kuifanya jumuiya nzima
kunung'unika dhidi ya Mose kwa kueneza
taarifa mbaya kuhusu hiyo nchi: 37 [d]watu
hawa waliohusika kueneza taarifa mbaya
kuhusu hiyo nchi walipigwa na kuanguka
kwa tauni mbele za BWANA. 38 [e]Miongoni
mwa watu waliokwenda kuipeleleza hiyo
nchi, ni Yoshua mwana wa Nuni, na Kalebu
mwana wa Yefune peke yao waliosalia.
39 [f]Mose alipotoa taarifa hii kwa Waisraeli
wote, walimboleza kwa uchungu.
40 [g]Mapema asubuhi siku iliyofuata
walipanda juu kuelekea kwenye nchi ya
vilima virefu, wakasema, "Tumetenda
dhambi. Tutakwea mpaka mahali BWANA
alipotuahidi."
41 [h]Lakini Mose akasema, "Kwa nini hamtii
amri ya BWANA? Jambo hili halitafanikiwa!
42 [i]Msipande juu, kwa kuwa BWANA hayupo
pamoja nanyi. Mtashindwa na adui zenu,
43 [j]kwa kuwa Waamaleki na Wakanaani
watapambana nanyi huko. Kwa sababu
mmemwacha BWANA, hatakuwa pamoja
nanyi, ninyi mtaanguka kwa upanga."
44 [k]Hata hivyo, kwa kiburi chao
walipanda juu kuelekea nchi ya vilima
virefu, ijapokuwa Mose hakutoka kambini
wala Sanduku la Agano la BWANA. 45 [l]Ndipo
Waamaleki na Wakanaani walioishi katika
hiyo nchi ya vilima wakateremka na
kuwashambulia, wakawapiga njia yote
hadi Horma.

### *Sadaka Za Nyongeza*

15 BWANA akamwambia Mose, 2 [m]"Sema
na Waisraeli uwaambie: 'Baada ya
ninyi kuingia katika nchi ninayowapa
kama nyumbani, 3 [n]nanyi mkitoa sadaka za
kuteketezwa kwa moto, kutoka makundi
ya ng'ombe au kondoo, kama harufu nzuri
inayompendeza BWANA, ikiwa ni sadaka
za kuteketezwa au dhabihu, kwa ajili ya
nadhiri maalum ama sadaka ya hiari au
sadaka ya sikukuu zenu, 4 [o]ndipo yeye
aletaye sadaka yake ataiweka mbele za
BWANA sadaka ya nafaka, sehemu ya kumi
ya efa[p] ya unga laini uliochanganywa na
robo ya hini[q] ya mafuta. 5 [r]Pamoja na kila
mwana-kondoo kwa ajili ya sadaka ya
kuteketezwa au dhabihu, andaa robo ya
hini ya divai kwa sadaka ya kinywaji.
6 [s]" 'Pamoja na kondoo dume andaa

[a]**14:34** Hes 13:25; 14:32, 33; Za 95:10; Eze 4:6; Za 77:8; Ebr 4:1
[b]**14:35** Hes 23:19
[c]**14:36** Hes 13:4-16, 32
[d]**14:37** Hes 13:32; 16:49; 25:9; 26:1; 31:16; 1Kor 10:10; Ebr 3:17; Kum 4:3
[e]**14:38** Hes 13:4-16; Yos 14:6
[f]**14:39** Kut 33:4; Mit 19:3; Mt 8:12; Ebr 12:17
[g]**14:40** Hes 13:17; Kut 9:27; Kum 1:41
[h]**14:41** 2Nya 24:20; Ay 9:4; Isa 59:1, 2; Yer 2:37
[i]**14:42** Kum 1:42
[j]**14:43** Amu 1:19; 6:16; 3:13; Hes 13:29; Mwa 39:23; Kum 21:8; Yos 6:27; 1Sam 3:19; 18:14; 2Nya 1:1
[k]**14:44** Kum 1:43; Hes 31:6
[l]**14:45** Hes 21:3; Kum 1:44; Yos 12:14; 15:30; 19:4; Amu 1:17; 1Sam 30:30; 1Nya 4:30
[m]**15:2** Law 23:10
[n]**15:3** Law 1:2, 9; 23:1-44; Hes 28:13; 7:16; Ezr 1:4; Kum 16:10; Mwa 8:21; Kut 29:18; 2Kor 2:15; Efe 5:2
[o]**15:4** Law 6:14; Kut 16:36; Law 14:10; Kut 29:40; Isa 66:20
[p]4 Sehemu ya kumi ya efa ni sawa na kilo moja.
[q]4 Robo ya hini ni sawa na lita moja.
[r]**15:5** Law 3:7; 10:9; Mwa 35:14; Hes 28:7, 14; Gal 3:28; Kol 3:11; Law 24:22
[s]**15:6** Law 5:15; 23:13; Hes 28:12; 29:14; Eze 46:14

sadaka ya nafaka ya sehemu mbili za kumi
za efa[a] za unga laini uliochanganywa na
theluthi moja[b] ya hini ya mafuta, 7 [c]na
theluthi moja ya hini ya divai kama sadaka
ya kinywaji. Vitoe kama harufu nzuri
inayompendeza BWANA.
8 [d]“ ‘Unapoandaa fahali mchanga kama
sadaka ya kuteketezwa au dhabihu, kwa
ajili ya nadhiri maalum au sadaka ya amani
kwa BWANA, 9 [e]leta pamoja na huyo fahali
sadaka ya nafaka ya unga laini sehemu tatu
za kumi za efa[f] uliochanganywa na nusu ya
hini[g] ya mafuta. 10 [h]Pia utaleta nusu ya hini
ya divai kama sadaka ya kinywaji. Itakuwa
sadaka iliyoteketezwa kwa moto, harufu
nzuri inayompendeza BWANA. 11 Kila fahali
au kondoo dume, kila mwana-kondoo au
mbuzi mchanga, atatayarishwa kwa njia
hii. 12 [i]Fanyeni hivi kwa ajili ya kila mmoja,
kwa kadiri ya wingi wa mtakavyoandaa.
13 [j]“ ‘Kila mmoja ambaye ni mzawa
ni lazima afanye vitu hivi kwa njia hii
hapo aletapo sadaka ya kuteketezwa kwa
moto kama harufu nzuri inayompendeza
BWANA. 14 [k]Kwa vizazi vijavyo, wakati
wowote mgeni au mtu mwingine yeyote
anayeishi miongoni mwenu aletapo sadaka
ya kuteketezwa kuwa harufu nzuri ya
kumpendeza BWANA, ni lazima afanye
sawasawa kabisa na jinsi mnavyofanya
ninyi. 15 [l]Jumuiya itakuwa na sheria hizo
hizo kwenu na kwa mgeni aishiye miongoni
mwenu; hii ni amri ya kudumu kwa vizazi
vijavyo. Ninyi na mgeni mtakuwa sawa
mbele za BWANA: 16 [m]Sheria hizo hizo na
masharti hayo hayo hayo, yatawahusu ninyi
na mgeni aishiye miongoni mwenu.’ ”
17 BWANA akamwambia Mose, 18 [n]“Sema
na Waisraeli na uwaambie: ‘Mtakapoingia
katika nchi ninayowapeleka 19 [o]nanyi mkala
chakula cha nchi hiyo, toeni sehemu ya
chakula hicho kama sadaka kwa BWANA.
20 [p]Toeni andazi kutoka kwa malimbuko
ya chakula chenu kitokacho katika ardhi,
na mkitoe kama sadaka kutoka sakafu ya
kupuria nafaka. 21 [q]Kwa vizazi vyote vijavyo
hamna budi kutoa sadaka hii kwa BWANA
kutoka kwa malimbuko ya unga wenu.

*Sadaka Kwa Ajili Ya Dhambi Isiyo Ya Makusudi*

22 [r]“ ‘Basi kama pasipo kukusudia
umeshindwa kushika mojawapo katika
amri hizi ambazo BWANA alimpa Mose,
23 amri yoyote ya BWANA kwenu kupitia
Mose, tangu siku ile BWANA alipowapa
na inaendelea hadi vizazi vyote vijavyo;
24 [s]ikiwa hili limefanyika pasipo kukusudia
bila jumuiya kuwa na habari nalo, basi
jumuiya yote itatoa fahali mchanga kuwa
sadaka ya kuteketezwa ikiwa harufu nzuri
inayompendeza BWANA, pamoja na sadaka
ya nafaka na ya kinywaji zilizoamriwa
kwayo, na mbuzi dume kwa ajili ya sadaka
ya dhambi. 25 [t]Kuhani atafanya upatanisho
kwa ajili ya jumuiya yote ya Kiisraeli,
nao watasamehewa, kwa kuwa haikuwa
makusudi nao wamemletea BWANA sadaka
iliyoteketezwa kwa moto na sadaka ya
dhambi kwa ajili ya kosa lao. 26 Jumuiya
yote ya Kiisraeli pamoja na wageni waishio
miongoni mwao watasamehewa, kwa
sababu watu wote walihusika katika kosa
lile lisilokusudiwa.

[a]6 Sehemu mbili za kumi za efa ni sawa na kilo 2.
[b]6 Theluthi moja ya hini ni sawa na lita moja na nusu.
[c]**15:7** Law 1:9; 23:13; Hes 28:14; 29:18
[d]**15:8** Kut 12:5; Law 1:5; 22:18; 3:6
[e]**15:9** Law 2:1; 14:10
[f]9 Sehemu tatu za kumi za efa ni sawa na kilo 3.
[g]9 Nusu ya hini ni sawa na lita 2.
[h]**15:10** Hes 28:14; Law 23:13; 1:9; Amu 2:17; Yer 3:2; 7:24; Hos 4:12; Eze 20:16
[i]**15:12** Ezr 7:17
[j]**15:13** Law 16:29; 1:9
[k]**15:14** Law 3:17; 22:18; Hes 10:8; Kut 12:19, 43; 22:21
[l]**15:15** Hes 9:14
[m]**15:16** Kut 12:49; Law 22:18; Hes 9:14
[n]**15:18** Law 23:10
[o]**15:19** Yos 5:11; 12; Hes 18:8
[p]**15:20** Law 23:14; Hes 18:2; Mwa 50:10; Kut 23:19; Neh 10:37; Mit 3:9; Law 2:14
[q]**15:21** Law 23:14; Eze 44:30; Rum 11:16
[r]**15:22** Law 4:2; 1Yn 2:1
[s]**15:24** Law 5:15; 4:14; 23:13; 4:3; Hes 6:15; Law 4:13, 23; Hes 28:15; Ezr 6:17; 8:35
[t]**15:25** Law 4:3, 20; Rum 3:25; Ebr 2:17; Rum 5; 11; Dan 9:24; Ebr 10:10-12

27 [a]“ ‘Lakini kama mtu mmoja peke
yake akitenda dhambi pasipo kukusudia,
ni lazima alete mbuzi mke wa mwaka
mmoja kwa ajili ya sadaka ya dhambi.
28 [b]Kuhani atafanya upatanisho mbele
za BWANA kwa ajili ya yule aliyekosa
kwa kufanya dhambi pasipo kukusudia,
upatanisho utakapofanywa kwa ajili
yake, atasamehewa. 29 [c]Sheria hiyo moja
itamhusu kila mmoja ambaye ametenda
dhambi pasipo kukusudia, awe Mwisraeli
mzawa ama mgeni.
30 [d]“ ‘Lakini yeyote ambaye amefanya
dhambi kwa dharau awe mzawa au
mgeni, anamkufuru BWANA, naye mtu
huyo ni lazima akatiliwe mbali na watu
wake. 31 [e]Kwa sababu amelidharau neno la
BWANA na kuvunja amri zake, mtu huyo ni
lazima akatiliwe mbali; hatia yake inabaki
juu yake.’ ”

*Mvunja Sabato Auawe*

32 [f]Waisraeli walipokuwa jangwani, mtu
mmoja alikutwa akikusanya kuni siku ya
Sabato. 33 Wale waliomkuta akikusanya
kuni wakamleta kwa Mose, Aroni na
kusanyiko lote, 34 [g]nao wakamweka
kifungoni, kwa sababu haikufahamika
kwa wazi kwamba afanyiwe nini. 35 [h]Ndipo
BWANA akamwambia Mose, “Huyo mtu ni
lazima afe. Kusanyiko lote lazima limpige
mawe nje ya kambi.” 36 [i]Hivyo kusanyiko
likamtoa nje ya kambi na kumpiga mawe
hadi akafa, kama BWANA alivyomwamuru
Mose.

*Vifundo Kwenye Mavazi*

37 BWANA akamwambia Mose, 38 [j]“Sema
na Waisraeli uwaambie: ‘Kwa vizazi vyote
vijavyo jifanyieni vifundo katika pindo za
mavazi yenu vikiwa na uzi wa buluu kwenye
kila kifundo. 39 [k]Mtakuwa mkivitazama
vifundo hivyo ili mpate kukumbuka amri
zote za BWANA, ili mpate kuzitii msije
mkajitia uzinzi wenyewe kwa kuzifuata
tamaa za mioyo yenu na za macho yenu.
40 [l]Ndipo mtakumbuka kuzitii amri zangu
zote nanyi mtawekwa wakfu kwa Mungu
wenu. 41 [m]Mimi Ndimi BWANA Mungu wenu,
niliyewatoa Misri niwe Mungu wenu. Mimi
Ndimi BWANA Mungu wenu.’ ”

*Kora, Dathani Na Abiramu*

16 [n]Kora mwana wa Ishari, mwana wa
Kohathi, mwana wa Lawi, pamoja na
baadhi ya Wareubeni, yaani Dathani na
Abiramu, wana wa Eliabu, na Oni mwana
wa Pelethi, wakachukua baadhi ya watu,
2 [o]wakainuka dhidi ya Mose. Pamoja nao
walikuwepo wanaume wa Kiisraeli 250,
watu waliojulikana, viongozi wa jumuiya
waliokuwa wameteuliwa kuwa wakuu
wa kusanyiko. 3 [p]Wakaja kama kikundi
kuwapinga Mose na Aroni, wakawaambia,
“Ninyi mmejitukuza sana! Kusanyiko hili
lote ni takatifu, kila mmoja wao, naye
BWANA yu pamoja nao. Kwa nini basi
mmejitukuza wenyewe juu ya kusanyiko
la BWANA?”
4 [q]Mose aliposikia jambo hili, akaanguka
kifudifudi. 5 [r]Kisha akamwambia Kora na

[a]**15:27** Law 4:3, 27; Hes 6:14; Za 19:13; Lk 12:48
[b]**15:28** Hes 8:12; 28:22; Law 4:20
[c]**15:29** Kut 12:49
[d]**15:30** Hes 14:40-44; Kum 1:43; 17:13; Za 19:13; 2Fal 19:6, 20; Isa 37:6, 23; Eze 20:27; Mwa 17:14; Ay 31:22
[e]**15:31** Hes 11:14; Mit 13:13; Za 119:126; 1Sam 15:23-26; 2Sam 11:27; 12:9; Eze 18:20
[f]**15:32** Hes 12:16; Kut 31:14-15; 35:2-3
[g]**15:34** Hes 9:8; Law 24:12
[h]**15:35** Kut 31:14-15; Law 20:2; Lk 4:29; Mdo 7:58
[i]**15:36** Law 20:2; Kut 31:14; Yer 17:21
[j]**15:38** Law 3:17; Hes 10:8; Kum 22:12; Mt 23:5
[k]**15:39** Kum 4:23; 6:12; Za 73:27; 78:37; 106:39; Law 17:7
[l]**15:40** Mwa 26:5; Kum 11:13; Za 103:18; 119:56; Law 11:44; Rum 12:1; Kol 1:22; 1Pet 1:15
[m]**15:41** Mwa 17:7; Kut 20:2
[n]**16:1** Kut 6:24; Yud 11; Za 106:17; Hes 26:8; Kum 11:6
[o]**16:2** Hes 27:3; 1:16; 26:9
[p]**16:3** Za 106:16; Kut 19:6; Hes 14:14; 12:2
[q]**16:4** Hes 14:2; 20:6
[r]**16:5** Law 10:3; 2Tim 2:19; Yer 30:21; Hes 17:5; Za 65:4; 105:26; Yer 50:44; Law 21:6-12; Kut 28:1; 1Sam 2:28; Eze 40:46

wafuasi wake wote: “Asubuhi BWANA
ataonyesha ni nani aliye wake na ni nani
aliye mtakatifu, tena atamtaka mtu huyo
aje kwake. Mtu yule ambaye atamchagua
atamfanya kuja karibu naye. 6 [a]Wewe Kora
na wafuasi wako wote mtafanya hivi:
Chukueni vyetezo, 7 [b]kesho wekeni moto
na uvumba kwenye hivyo vyetezo mbele za
BWANA. Mtu ambaye BWANA atamchagua
atakuwa ndiye mtakatifu. Ninyi Walawi
mmejitukuza sana!”
8 Pia Mose akamwambia Kora, “Enyi
Walawi! Sasa nisikilizeni. 9 [c]Haiwatoshi
ninyi kwamba Mungu wa Israeli amewateua
ninyi kutoka kusanyiko lote la Kiisraeli, na
kuwaleta karibu naye mpate kufanya kazi
kwenye Maskani ya BWANA, na kusimama
mbele ya kusanyiko ili kuwahudumia?
10 [d]Amekuleta wewe na ndugu zako Walawi
mwe karibu naye, lakini sasa unajaribu
kupata na ukuhani pia. 11 [e]Wewe na wafuasi
wako wote mmekusanyika pamoja kinyume
cha BWANA. Aroni ni nani kwamba ninyi
mnung’unike dhidi yake?”
12 Kisha Mose akawaita Dathani na
Abiramu, wana wa Eliabu. Lakini wao
wakasema, “Sisi hatuji! 13 [f]Haitoshi tu
kwamba wewe umetuleta kutoka nchi
itiririkayo maziwa na asali ili kutuua
sisi jangwani? Nawe sasa pia unataka
kuwa mkuu juu yetu? 14 [g]Zaidi ya hayo,
hujatuingiza katika nchi inayotiririka
maziwa na asali, wala hujatupa urithi wa
mashamba na mashamba ya mizabibu. Je,
utayang’oa macho ya watu hawa? Hapana,
sisi hatuji!”
15 [h]Ndipo Mose akakasirika sana na
kumwambia BWANA, “Usiikubali sadaka
yao. Mimi sikuchukua chochote, hata punda
kutoka kwao, wala sijamkosea hata mmoja
wao.”
16 Mose akamwambia Kora, “Wewe na
wafuasi wako wote kesho mtatokea mbele
za BWANA: yaani wewe na hao wenzako,
pamoja na Aroni. 17 [i]Kila mtu atachukua
chetezo chake na kuweka uvumba ndani
yake, vyetezo 250 kwa jumla, na kukileta
mbele za BWANA. Wewe na Aroni mtaleta
vyetezo vyenu pia.” 18 Kwa hiyo kila mtu
akachukua chetezo chake, akaweka moto
na uvumba ndani yake, na kusimama
pamoja na Mose na Aroni kwenye mlango
wa Hema la Kukutania. 19 [j]Kora alipokuwa
amekusanya wafuasi wake wote kuwapinga
Mose na Aroni kwenye mlango wa Hema
la Kukutania, utukufu wa BWANA ukatokea
kwa kusanyiko lote. 20 BWANA akamwambia
Mose na Aroni, 21 [k]“Jitengeni kutoka kwenye
kusanyiko hili ili nipate kuwaangamiza
mara moja.”
22 [l]Lakini Mose na Aroni wakaanguka
kufudifudi na kulia kwa sauti, wakasema,
“Ee Mungu, Mungu wa roho za wanadamu
wote, utakuwa na hasira na kusanyiko
lote wakati ni mtu mmoja tu ametenda
dhambi?”
23 Ndipo BWANA akamwambia Mose,
24 “Liambie kusanyiko, ‘Ondokeni hapo
karibu na mahema ya Kora, Dathani na
Abiramu.’ ”
25 [m]Mose akainuka na kuwaendea
Dathani na Abiramu, nao wazee wa Israeli
wakafuatana naye. 26 [n]Mose akalionya
kusanyiko, “Sogeeni nyuma mbali na

---

[a]**16:6** Law 10:1; Ufu 8:3
[b]**16:7** Law 10:1; Kut 30:9
[c]**16:9** Mwa 30:15; Hes 3:6; Kum 10:8; 17:12; 21:5; 1Sam 2:11; Za 134:1; Eze 44:11; 1Sam 18:23; Isa 7:13
[d]**16:10** Hes 3:10; 18:7; Amu 17:5, 12
[e]**16:11** 1Kor 10:10; Kut 16:7-8; 1Kor 3:5
[f]**16:13** Hes 13:27; 14:2; Mwa 13:8; Mdo 7:27, 35; Kut 2:14; Mdo 7:27, 35
[g]**16:14** Law 20:24; Kut 22:5; 23:11; Hes 20:5; 1Fal 4:25; Neh 13:15; Za 105:33; Yer 5:17; Hos 2:12; Yoe 2:22; Hag 2:19; Zek 3:10; Amu 16:21; 1Sam 2:11
[h]**16:15** Kut 4:14; 1Sam 12:3; Mdo 20:33; 2Kor 7:2
[i]**16:17** Eze 8:11
[j]**16:19** Hes 14:10; 20:2, 6; Kut 16:7; Law 9:6, 23
[k]**16:21** Mwa 19:14; Kut 32:10; Yer 51:6; Mdo 2:40; Ufu 18:4; Za 73:19
[l]**16:22** Hes 14:5; 27:16; Ay 12:10; 21:20; 27:8; 33:4; 34:14; Yer 32:27; Eze 18:4; Ebr 12:9; Mwa 18:23
[m]**16:25** Kut 19:7
[n]**16:26** Isa 52:11; Mwa 19:15; Yer 51:6; Mwa 19:12; Mdo 2:40; 2Kor 6:17; Ufu 18:4

mahema ya hawa watu waovu! Msiguse
kitu chochote kilicho mali yao, la sivyo
mtafagiliwa mbali kwa sababu ya dhambi
zao zote.” 27 [a]Hivyo wakaondoka karibu
na mahema ya Kora, Dathani na Abiramu.
Dathani na Abiramu walikuwa wametoka
nje, nao walikuwa wamesimama pamoja na
wake zao, watoto wao na wale wanyonyao
kwenye mlango wa mahema yao.
28 [b]Ndipo Mose akasema, “Hivi ndivyo
mtakavyojua kuwa BWANA amenituma
kufanya mambo haya, na kwamba halikuwa
wazo langu. 29 [c]Ikiwa watu hawa watakufa
kifo cha kawaida na kupatwa na yale ya
kawaida yanayowapata wanadamu, basi
BWANA hakunituma mimi. 30 [d]Lakini ikiwa
BWANA ataleta jambo jipya kabisa, ardhi
ikifunua kinywa chake na kuwameza
wao, pamoja na kila kitu kilicho mali
yao, nao washuke chini kaburini[e] wakiwa
hai, ndipo mtafahamu kuwa watu hawa
wamemdharau BWANA.”
31 [f]Mara Mose alipomaliza kusema
haya yote, ardhi iliyokuwa chini yao
ikapasuka, 32 [g]nchi ikafunua kinywa chake
na kuwameza wao, pamoja na jamaa zao,
na watu wote wa Kora na mali zao zote.
33 [h]Wakashuka chini kaburini wakiwa hai,
pamoja na kila kitu walichokuwa nacho;
nchi ikajifunika juu yao, nao wakaangamia
wakatoweka kutoka kusanyiko. 34 Kutoka
kilio chao, Waisraeli wote waliowazunguka
walikimbia, wakipaza sauti, “Nchi
inatumeza na sisi pia!”

[a]**16:27** Yos 7:24; Isa 13:16; 14:21; Kut 33:8; Ay 9:4; Mit 16:18
[b]**16:28** 1Fal 18:36; Kut 3:12; Yn 5:36; 6:38; Kum 18:22; Zek 2:9; Yer 23:16; Eze 13:17
[c]**16:29** Hes 24:13; Ay 31:2; Mhu 3:19; Isa 10:3; Yer 5:9; Mao 4:22
[d]**16:30** Za 9:17; 16:10; 55:15; 141:7; Isa 5:14; 14:11; 38:18; Mwa 37:35; 1Sam 2:6; Ay 5:26; 21:13; Hes 14:11; Eze 26:20
[e]30 Kaburini hapa maana yake ni Kuzimu, kwa Kiebrania ni Sheol.
[f]**16:31** Isa 64:1-2; Eze 47:1-2; Mik 1:3-4; Zek 14:4
[g]**16:32** Kut 15:12; Za 10:17; 1Nya 6:22
[h]**16:33** Mhu 9:10

35 [i]Moto ukaja kutoka kwa BWANA,
ukawateketeza wale watu 250 waliokuwa
wakifukiza uvumba.
36 BWANA akamwambia Mose,
37 [j]“Mwambie Eleazari mwana wa kuhani
Aroni, atoe vyetezo kwenye mabaki
ya moto na kutawanya makaa mbali
kiasi, kwa maana vyetezo ni vitakatifu:
38 [k]vyetezo vya watu waliofanya dhambi
iliyowagharimu maisha yao. Fua vyetezo
hivyo kuwa bamba ili kufunika madhabahu,
kwa maana vimeletwa mbele za BWANA na
vimekuwa vitakatifu. Navyo viwe ishara
kwa Waisraeli.”
39 [l]Hivyo kuhani Eleazari akavikusanya
vile vyetezo vya shaba vilivyoletwa na wale
waliokuwa wameteketezwa kwa moto, naye
akavifua kufunika madhabahu, 40 [m]kama vile
BWANA alivyomwelekeza kupitia Mose. Hili
lilikuwa kuwakumbusha Waisraeli kwamba
hakuna mtu hata mmoja, isipokuwa mzao
wa Aroni, awezaye kuja kufukiza uvumba
mbele za BWANA, la sivyo, angekuwa kama
Kora na wafuasi wake.
41 [n]Siku iliyofuata jumuiya yote ya
Kiisraeli wakanung’unika dhidi ya Mose
na Aroni, wakisema, “Mmewaua watu wa
BWANA.”
42 [o]Lakini wakati kusanyiko
lilipokusanyika kupingana na Mose na
Aroni, nalo likageuka kuelekea Hema la
Kukutania, ghafula wingu likafunika Hema,
nao utukufu wa BWANA ukatokea. 43 Ndipo
Mose na Aroni wakaenda mbele ya Hema
la Kukutania, 44 naye BWANA akamwambia
Mose, 45 [p]“Jitenge mbali na kusanyiko hili
ili niweze kuwaangamiza mara moja.”
Wakaanguka chini kifudifudi.

[i]**16:35** Hes 11:1-3; 26:10; Ufu 11:5; Law 10:2; Za 106:18
[j]**16:37** Kut 6:23
[k]**16:38** Law 10:1; Mit 20:2; Kut 20:24; 38:1-7; Hes 26:10; Kum 28:46; Yer 44:29; Eze 14:8; 2Pet 2:6
[l]**16:39** 2Nya 26:18; Law 20:14
[m]**16:40** Kut 30:1, 9; Isa 1:13; 66:3; Yer 41:5; 44:3; 2Nya 26:18; Hes 3:10
[n]**16:41** Hes 14:2; Za 106:13; Mdo 21:28
[o]**16:42** Kut 16:7; Hes 14:10; 20:6; Law 9:23
[p]**16:45** Kut 32:10; 1Nya 16:21; Mt 26:39

46 [a]Kisha Mose akamwambia Aroni, "Chukua chetezo chako na uweke uvumba ndani yake, pamoja na moto kutoka madhabahuni, nawe uende haraka kwenye kusanyiko ili kufanya upatanisho kwa ajili yao. Ghadhabu imekuja kutoka kwa BWANA, na tauni imeanza." 47 [b]Hivyo Aroni akafanya kama Mose alivyosema, akakimbilia katikati ya kusanyiko. Tauni ilikuwa tayari imeanza miongoni mwa watu, lakini Aroni akafukiza uvumba na kufanya upatanisho kwa ajili yao. 48 [c]Aroni akasimama kati ya waliokuwa hai na waliokufa, nayo tauni ikakoma. 49 Lakini walikufa watu 14,700 kutokana na tauni hiyo, licha ya wale waliokuwa wamekufa kwa sababu ya Kora. 50 Ndipo Aroni akamrudia Mose kwenye mlango wa Hema la Kukutania, kwa maana tauni ilikuwa imekoma.

### *Kuchipuka Kwa Fimbo Ya Aroni*

17 BWANA akamwambia Mose, 2 [d]"Sema na Waisraeli, na ujipatie fimbo kumi na mbili kutoka kwao, moja kutoka kwa kila mmoja wa viongozi wa kabila za baba zao. Andika jina la kila mtu kwenye fimbo yake. 3 [e]Kwenye fimbo ya Lawi andika jina la Aroni, kwa maana ni lazima iwepo fimbo moja kwa kila kiongozi kwa ajili ya kila kabila la baba zao. 4 [f]Ziweke hizo fimbo ndani ya Hema la Kukutania mbele ya Sanduku la Ushuhuda, mahali nikutanapo nawe. 5 [g]Fimbo ya mtu nitakayemchagua itachipuka, nami mwenyewe nitayakomesha haya manung'uniko ya mara kwa mara ya Waisraeli dhidi yako."

6 Hivyo Mose akasema na Waisraeli, nao viongozi wao wakampa fimbo kumi na mbili, fimbo moja kwa ajili ya kila kabila la baba zao, nayo fimbo ya Aroni ikiwa miongoni mwa hizo. 7 [h]Mose akaziweka hizo fimbo mbele za BWANA ndani ya Hema la Ushuhuda.

8 [i]Siku iliyofuata Mose aliingia kwenye Hema la Ushuhuda akaona ile fimbo ya Aroni ambayo iliwakilisha jamaa ya Lawi haikuwa tu imechipuka, bali pia ilikuwa imetoa machipukizi, kuchanua maua na kuzaa malozi. 9 Ndipo Mose akaleta zile fimbo zote kwa Waisraeli wote kutoka mbele za BWANA. Wakaziangalia, na kila mtu akaichukua fimbo yake mwenyewe.

10 [j]BWANA akamwambia Mose, "Rudisha fimbo ya Aroni mbele ya Sanduku la Ushuhuda, ili ihifadhiwe kama alama kwa waasi. Hili litakomesha manung'uniko yao dhidi yangu, ili kwamba wasife." 11 Mose akafanya kama BWANA alivyomwamuru.

12 [k]Waisraeli wakamwambia Mose, "Tutakufa! Tumepotea, sote tumepotea! 13 [l]Yeyote akaribiaye Maskani ya BWANA atakufa. Je, sisi sote tutakufa?"

### *Wajibu Wa Makuhani Na Walawi*

18 [m]BWANA akamwambia Aroni, "Wewe, wanao na jamaa ya baba yako mtawajibika kwa makosa dhidi ya mahali patakatifu, na wewe na wanao peke yenu ndio mtakaowajibika kwa makosa dhidi ya ukuhani. 2 [n]Walete Walawi wenzako kutoka kabila la baba zako ili waungane nanyi na kuwasaidia wakati wewe na wanao mnapohudumu mbele ya Hema la Ushuhuda. 3 [o]Watawajibika kwenu na watafanya kazi zote za Hema, lakini kamwe wasisogelee vifaa vya patakatifu au madhabahu, la sivyo wao na ninyi mtakufa. 4 [p]Watajiunga nanyi na watawajibika kwa utunzaji wa Hema la Kukutania, yaani kazi zote kwenye Hema, wala hakuna mtu

[a]**16:46** Law 10:1-6; 26:25; Kut 29:36; Hes 1:53; 8:19; Za 106:29; Yos 7:1; 22:18; 1Sam 6:19; 2Sam 24:1; 1Nya 17:24
[b]**16:47** Hes 25:6-8
[c]**16:48** Hes 25:8; Za 106:30; 2Sam 24:16-17; Ay 33:24; Yak 5:16; 1The 1:10; Ebr 7:24
[d]**17:2** Mwa 32:10; Kut 4:2; Hes 1:4
[e]**17:3** Hes 1:3
[f]**17:4** Kut 1:3; 16:34; 25:22
[g]**17:5** Hes 16:5; Kut 16:7
[h]**17:7** Kut 38:21; Mdo 7:44
[i]**17:8** Hes 1:50; Eze 17:24; Ebr 9:4
[j]**17:10** Kut 23:21; Za 66:7; 68:18; Mit 24:21
[k]**17:12** Amu 13:22; Isa 6:5; 15:1
[l]**17:13** Hes 1:51
[m]**18:1** Kut 28:38
[n]**18:2** Hes 3:10
[o]**18:3** Hes 3:32; 1:51
[p]**18:4** Hes 3:34

mwingine yeyote atakayeweza kusogea
karibu hapo mlipo.
5 [a]“Mtawajibika katika utunzaji wa mahali
patakatifu na madhabahu, ili kwamba
ghadhabu isiwaangukie Waisraeli tena.
6 [b]Mimi mwenyewe nimewachagua Walawi
wenzenu kutoka miongoni mwa Waisraeli
kama zawadi kwenu, waliowekwa wakfu
kwa BWANA ili kufanya kazi katika Hema
la Kukutania. 7 [c]Lakini ni wewe tu na wanao
mtakaoweza kutumika kama makuhani
kuhusiana na kila kitu kwenye madhabahu
na ndani ya pazia. Ninawapa utumishi wa
ukuhani kama zawadi. Mtu mwingine
yeyote atakayekaribia mahali patakatifu
ni lazima auawe.”

*Sadaka Kwa Ajili Ya Makuhani Na Walawi*

8 [d]Kisha BWANA akamwambia Aroni,
“Mimi mwenyewe nimekuweka kuwa
mwangalizi wa sadaka zote zitakazotolewa
kwangu; matoleo yote matakatifu
Waisraeli wanayonipa ninakupa wewe
na wanao kama sehemu yenu na fungu
lenu la kawaida. 9 [e]Mtachukua sehemu
ya yale matoleo matakatifu sana ambayo
hayateketezwi kwa moto. Kutoka kwa
matoleo yote wanayoniletea kama sadaka
takatifu sana, ziwe za nafaka, au za dhambi,
au za makosa, sehemu ile itakuwa yako
na wanao. 10 [f]Mtaila kama kitu kilicho
kitakatifu sana; kila mwanaume ataila. Ni
lazima mtaiheshimu kama takatifu.
11 [g]“Hiki pia ni chako: chochote
kilichotengwa kutoka kwenye matoleo
yote ya sadaka za kuinuliwa za Waisraeli.
Ninakupa wewe haya, wana na binti zako
kama sehemu yenu ya kawaida. Kila mmoja
wa nyumba yako ambaye ni safi kwa
taratibu za ibada anaweza kuyala.
12 [h]“Ninawapa mafuta ya zeituni yaliyo
bora kuliko yote, na divai mpya iliyo
bora kuliko zote na nafaka wanazompa
BWANA kama malimbuko katika mavuno
yao. 13 [i]Malimbuko yote ya nchi ambayo
wanamletea BWANA yatakuwa yenu. Kila
mmoja nyumbani kwako ambaye ni safi
kwa taratibu za Ibada anaweza kula.
14 [j]“Kila kitu katika Israeli ambacho
kimetolewa kwa BWANA ni chenu. 15 [k]Kila
mzaliwa wa kwanza wa mwanadamu na wa
mnyama, ambaye ametolewa kwa BWANA
ni wenu. Lakini ni lazima mtamkomboa kila
mwana mzaliwa wa kwanza na kila mzaliwa
wa kwanza wa kiume wa wanyama wasio
safi. 16 [l]Watakapokuwa na umri wa mwezi
mmoja, ni lazima mtawakomboa kwa bei
ya ukombozi iliyowekwa, kwa shekeli tano[m]
za fedha, kulingana na shekeli ya mahali
patakatifu, yenye uzito wa gera ishirini.[n]
17 [o]“Lakini kamwe usimkomboe mzaliwa
wa kwanza wa maksai, kondoo au mbuzi;
hawa ni watakatifu. Nyunyizia damu yao
juu ya madhabahu na uchome mafuta
yao kama sadaka itolewayo kwa moto,
harufu nzuri inayompendeza BWANA.
18 [p]Nyama zao zitakuwa chakula chenu,
kama ilivyokuwa kidari cha kuinuliwa
na paja la mguu wa kulia. 19 [q]Chochote
kitakachotengwa kutoka sadaka takatifu
ambazo Waisraeli wanamtolea BWANA,
ninakupa wewe, wanao na binti zako kama
fungu lenu la kawaida. Ni Agano la milele la
chumvi mbele za BWANA kwako na watoto
wako.”

---

[a]**18:5** Law 6:12
[b]**18:6** Hes 3:8-9
[c]**18:7** Ebr 9:3, 6; Kut 29:9; 40:13; Ebr 5:4; Hes 3:10
[d]**18:8** Law 2:2; 6:16; 7:6, 31-34; Kum 18:1; 2Nya 31:4
[e]**18:9** Law 6:17; 2:1; 6:25; 5:15
[f]**18:10** Law 6:16; 6:17-18
[g]**18:11** Kut 29:26; Law 7:30; Hes 6:20; Law 7:31-34; 13:3; 22:1-16
[h]**18:12** Kum 7:13; 11:14; 12:17; 28:51; 2Fal 18:32; 2Nya 31:5; Neh 10:35, 37; Law 23:19; Kut 34:26
[i]**18:13** Kut 29:27
[j]**18:14** Law 27:21; Yos 6:17-19
[k]**18:15** Kut 13:2; Hes 3:46; Mwa 10:15; Kut 13:13
[l]**18:16** Hes 3:15; Law 27:6; Kut 30:13; Hes 3:47
[m]16 Shekeli tano za fedha ni sawa na gramu 55.
[n]16 Gera 20 ni sawa na gramu 55.
[o]**18:17** Law 27:4; 3:2; Kut 29:13; Law 1:4
[p]**18:18** Law 7:30
[q]**18:19** 2Fal 12:4; Law 2:13

20 [a]BWANA akamwambia Aroni,
“Hutakuwa na urithi wowote katika nchi
yao, wala hutakuwa na sehemu miongoni
mwao; Mimi ni fungu lako na urithi wako
miongoni mwa Waisraeli.

21 [b]“Ninawapa Walawi zaka yote katika
Israeli kama urithi wao kuwa kama
malipo kwa kazi wanayoifanya wakati
wanapohudumu katika Hema la Kukutania.
22 [c]Kuanzia sasa, kamwe Waisraeli
wasisogelee karibu na Hema la Kukutania,
la sivyo watabeba matokeo ya dhambi zao,
nao watakufa. 23 [d]Ni Walawi watakaofanya
kazi katika Hema la Kukutania na kubeba
wajibu wa makosa dhidi yake. Hili ni
agizo la kudumu kwa vizazi vijavyo.
Hawatapokea urithi wowote miongoni
mwa Waisraeli. 24 [e]Badala yake, ninawapa
Walawi zaka zote zinazotolewa na Waisraeli
kama sadaka kwa BWANA kuwa urithi wao.
Hiyo ndiyo sababu nimesema hivi kuhusu
wao: ‘Hawatakuwa na urithi miongoni mwa
Waisraeli.’ ”

25 BWANA akamwambia Mose, 26 [f]“Sema
na Walawi na uwaambie: ‘Mtakapopokea
zaka kutoka kwa Waisraeli ambayo
ninawapa kama urithi wenu kutoka kwao,
ni lazima mtoe sehemu ya kumi ya hiyo
zaka kama sadaka kwa BWANA, iwe zaka
ya hiyo zaka. 27 [g]Sadaka yenu itahesabiwa
kwenu kama nafaka kutoka sakafu ya
kupuria, au divai kutoka kwenye shinikizo
la kukamulia zabibu. 28 [h]Kwa njia hii, ninyi
pia mtatoa sadaka kwa BWANA kutoka zaka
zote mtakazopokea kutoka kwa Waisraeli.
Kutoka kwenye zaka hizi, ni lazima mtoe
sehemu ya BWANA kwa Aroni, kuhani. 29 Ni
lazima mtoe kama sehemu ya BWANA iliyo
nzuri sana tena ile sehemu iliyo takatifu
sana kuliko zote ya kile kitu mlichopewa.’

30 “Waambie Walawi: ‘Mtakapotoa
sehemu zilizo bora sana, itahesabiwa
kwenu kama mazao ya sakafu ya kupuria
nafaka, au ya shinikizo la kukamulia
zabibu. 31 Ninyi na watu wa nyumbani
mwenu mnaweza kula sehemu iliyobaki
mahali popote, kwani ndio ujira wenu kwa
ajili ya kazi yenu katika Hema la Kukutania.
32 [i]Kwa kutoa sehemu zake zilizo bora sana,
hamtakuwa na hatia katika jambo hili;
ndipo hamtatia unajisi sadaka takatifu za
Waisraeli, nanyi hamtakufa.’ ”

*Maji Ya Utakaso*

19 BWANA akamwambia Mose na Aroni:
2 [j]“Hivi ndivyo sheria ambayo BWANA
ameagiza itakavyo: Waambie Waisraeli
wakuletee mtamba mwekundu asiye na
dosari wala waa, na ambaye hajapata
kufungwa nira. 3 [k]Mpeni kuhani Eleazari
huyo mtamba; naye atatolewa nje ya
kambi na kuchinjwa mbele yake huyo
kuhani. 4 [l]Kisha kuhani Eleazari atachukua
baadhi ya damu yake kwenye kidole
chake na kuinyunyiza mara saba kuelekea
upande wa mbele ya Hema la Kukutania.
5 [m]Wakati angali akitazama, mtamba huyo
atateketezwa: ngozi yake, nyama yake,
damu na sehemu zake za ndani. 6 [n]Kuhani
atachukua kuni za mti wa mwerezi, hisopo
na sufu nyekundu, na kuvitupa kwenye
huyo mtamba anayeungua. 7 [o]Baada ya
hayo, kuhani lazima afue nguo zake, na
aoge mwili wake kwa maji. Kisha anaweza
kurudi kambini, lakini atakuwa najisi
kwa kawaida ya ibada mpaka jioni. 8 Mtu
amchomaye huyo mtamba lazima naye pia
afue nguo zake na kuoga kwa maji, naye
pia atakuwa najisi mpaka jioni.

---

[a]**18:20** Hes 26:62; Kum 12:12; 10:9; 14:27; 18:1-2; Yos 13:33; Eze 44:28
[b]**18:21** Mwa 28:22; Hes 31:28; Kum 14:22; Neh 10:33; 13:5; Mal 3:8; Law 27:30-33; Ebr 7:5; Hes 1:53
[c]**18:22** Kut 28:43
[d]**18:23** Kut 12:14; 27:21; Hes 10:8; 26:62; Kum 10:9; Eze 44:10
[e]**18:24** Law 27:30; Kum 26:12
[f]**18:26** Neh 10:38
[g]**18:27** Law 7:18; Mwa 50:10; Kum 15:14; Amu 6:37; Rut 3:3, 6, 14; 1Sam 23:1
[h]**18:28** Mal 3:8
[i]**18:32** Law 22:15; 19:8
[j]**19:2** Mwa 15:9; Ebr 9:13; Law 22:19-25; Kum 21:3; 1Sam 6:7
[k]**19:3** Hes 3:4; Kut 29:14
[l]**19:4** Law 4:17
[m]**19:5** Kut 29:14
[n]**19:6** Za 51:7; Law 14:4
[o]**19:7** Law 11:25; 14:8

9 [a]“Mtu ambaye ni safi atakusanya majivu
ya mtamba huyo na kuyaweka mahali
ambapo ni safi nje ya kambi kwa taratibu
za kiibada. Yatahifadhiwa na jumuiya ya
Kiisraeli kwa matumizi katika maji ya
utakaso; ni kwa ajili ya kutakasa kutoka
dhambini. 10 [b]Mtu akusanyaye majivu ya
huyo mtamba ni lazima pia afue nguo
zake, kadhalika naye pia atakuwa najisi
hadi jioni. Hili litakuwa agizo la kudumu
kwa Waisraeli na kwa wageni wanaoishi
miongoni mwao.
11 [c]“Mtu yeyote agusaye maiti ya mtu
yeyote atakuwa najisi kwa siku saba. 12 [d]Ni
lazima ajitakase mwenyewe kwa maji katika
siku ya tatu na siku ya saba, ndipo atakuwa
safi. Lakini kama hatajitakasa mwenyewe
katika siku ya tatu na ya saba, hatakuwa
safi. 13 [e]Mtu yeyote agusaye maiti ya mtu
yeyote na kushindwa kujitakasa mwenyewe
hunajisi Maskani ya BWANA. Mtu huyo ni
lazima akatiliwe mbali na Israeli. Kwa
sababu hajanyunyiziwa maji ya utakaso,
yeye ni najisi; unajisi wake unabaki juu
yake.
14 “Hii ndiyo sheria itumikayo wakati mtu
amekufa ndani ya hema: Yeyote aingiaye
ndani ya hema hilo na yeyote aliye ndani
yake watakuwa najisi kwa muda wa siku
saba, 15 [f]nacho kila chombo kisicho na
kifuniko juu yake kitakuwa najisi.
16 [g]“Mtu yeyote aliyeko nje mahali pa
wazi agusaye mtu aliyeuawa kwa upanga
au mtu aliyekufa kwa kifo cha kawaida,
au mtu yeyote agusaye mfupa wa mtu
aliyekufa au kaburi, atakuwa najisi kwa
siku saba.
17 [h]“Kwa mtu aliye najisi, weka majivu
ya sadaka ya utakaso wa dhambi ndani ya
chombo, umimine maji safi juu yao. 18 [i]Kisha
mtu aliye safi kwa kawaida za kiibada
atachukua hisopo, achovye ndani ya maji,
na kunyunyizia hema na vifaa vyote pamoja
na watu ambao walikuwamo. Pia ni lazima
amnyunyizie mtu yeyote ambaye amegusa
mfupa wa mtu aliyekufa, au kaburi, au mtu
ambaye ameuawa, au mtu ambaye amekufa
kifo cha kawaida. 19 [j]Mtu ambaye ni safi
ndiye atakayemnyunyizia yeyote ambaye
ni najisi siku ya tatu na siku ya saba, na
katika siku ya saba atamtakasa mtu huyo.
Mtu ambaye ametakaswa lazima afue
nguo zake na kuoga kwa maji, na jioni ile
atakuwa safi. 20 [k]Lakini ikiwa mtu ambaye
ni najisi hakujitakasa mwenyewe, ni lazima
akatiliwe mbali na jumuiya, kwa sababu
ameinajisi Maskani ya BWANA. Maji ya
utakaso hayajanyunyizwa juu yake, naye
ni najisi. 21 [l]Hii ni sheria ya kudumu kwao.
“Mtu yeyote ambaye ananyunyiza yale
maji ya utakaso lazima pia afue nguo
zake, na yeyote ambaye hugusa maji ya
utakaso atakuwa najisi mpaka jioni. 22 [m]Kitu
chochote anachogusa mtu aliye najisi
kitakuwa najisi, na yeyote akigusaye huwa
najisi mpaka jioni.”

### *Maji Kutoka Kwenye Mwamba*

**(Kutoka 17:1-7)**

20 [n]Katika mwezi wa kwanza jumuiya
yote ya Kiisraeli ilifika kwenye Jangwa
la Sini, nao wakakaa Kadeshi. Miriamu
akafa huko na kuzikwa.
2 [o]Mahali hapo hapakuwa na maji kwa
ajili ya jumuiya hiyo, nao wakakusanyika
ili kumpinga Mose na Aroni. 3 [p]Watu
wakagombana na Mose, na kusema,
“Laiti tungelikufa wakati ndugu zetu

[a]**19:9** Ebr 9:13; Kut 29:31; Law 4:12; Hes 8:1; Mwa 35:2
[b]**19:10** Law 15:10; 14:46; 3:17; 22:18
[c]**19:11** Law 21:1; 8:33; Hes 31:19
[d]**19:12** Hes 31:19; 2Nya 26:21
[e]**19:13** Law 21:11; 15:31; 2Nya 36:14; Za 79:1; Law 22:3; 7:20; Hag 2:13
[f]**19:15** Law 6:28
[g]**19:16** Hes 31:19; 1Fal 13:2; 2Fal 23:14; Eze 6:5; 2Fal 23:6; Mt 23:27; Law 5:3
[h]**19:17** Hes 8:7
[i]**19:18** Kut 12:22; Law 4:17
[j]**19:19** Law 16:14-15; Hes 31:19; Eze 36:25; Ebr 10:22; Mwa 35:2
[k]**19:20** Za 14:7; Law 15:31; 14:8
[l]**19:21** Kut 27:21
[m]**19:22** Law 5:2; 15:4-12
[n]**20:1** Hes 13:21; 13:26; 33:36; Kum 1:46; Amu 11:17; Za 29:8; Kut 15:20
[o]**20:2** Kut 15:22; 17:1; Hes 16:19
[p]**20:3** Mwa 13:7; Kut 17:2; 21:18; 5:21; Hes 14:2; 16:31-35

walipoanguka na kufa mbele za Bwana!
4 [a]Kwa nini mmeileta jumuiya ya Bwana
kwenye jangwa hili, ili tufe humu, sisi na
mifugo yetu? 5 [b]Kwa nini mmetupandisha
kutoka Misri mpaka mahali hapa pa kutisha?
Hapa hakuna nafaka wala tini, zabibu au
makomamanga. Wala hapa hakuna maji
ya kunywa!"
6 [c]Mose na Aroni wakaondoka pale kwenye
kusanyiko mpaka kwenye mlango wa Hema
la Kukutania na kuanguka kifudifudi, nao
utukufu wa Bwana ukawatokea. 7 Bwana
akamwambia Mose, 8 [d]"Chukua ile fimbo,
na wewe na ndugu yako Aroni mkusanye
kusanyiko pamoja. Nena na ule mwamba
mbele ya macho yao, nao utatoa maji yake.
Utatoa maji kutoka huo mwamba kwa ajili
ya jumuiya ili wao na mifugo yao waweze
kunywa."
9 [e]Kwa hiyo Mose akaichukua hiyo fimbo
kutoka pale ilipokuwa mbele za Bwana
kama alivyomwagiza. 10 [f]Mose na Aroni
wakakusanya kusanyiko pamoja mbele ya
huo mwamba, naye Mose akawaambia,
"Sikilizeni, enyi waasi. Je, ni lazima
tuwatoleeni maji kutoka mwamba huu?"
11 [g]Ndipo Mose akainua mkono wake na
kuupiga mwamba mara mbili kwa fimbo
yake. Maji yakabubujika, nayo jumuiya na
mifugo yao wakanywa.
12 [h]Lakini Bwana akamwambia Mose na
Aroni, "Kwa sababu hamkuniamini mimi
kiasi cha kuniheshimu kama mtakatifu
machoni pa Waisraeli, hamtaiingiza
jumuiya hii katika nchi ninayowapa."
13 [i]Haya yalikuwa maji ya Meriba,[j] mahali
pale ambapo Waisraeli waligombana na
Bwana, naye akajionyesha mwenyewe
huko kuwa mtakatifu katikati yao.

*Edomu Wakatalia Israeli Kupita*

14 [k]Mose akawatuma wajumbe kutoka
Kadeshi kwenda kwa mfalme wa Edomu,
akisema:

"Hili ndilo ndugu yako Israeli
asemalo: Wewe unafahamu juu
ya taabu zote ambazo zimetupata.
15 [l]Baba zetu walishuka Misri, nasi
tumeishi huko miaka mingi. Wamisri
walitutesa sisi na baba zetu, 16 [m]lakini
tulipomlilia Bwana, alisikia kilio
chetu na akamtuma malaika akatutoa
Misri.

"Sasa tupo hapa Kadeshi, mji ulio
mpakani mwa nchi yako. 17 [n]Tafadhali
turuhusu tupite katika nchi yako.
Hatutapita katika shamba lolote,
wala shamba la mizabibu, au kunywa
maji kutoka kwenye kisima chochote.
Tutasafiri kufuata njia kuu ya mfalme,
na hatutageuka kulia wala kushoto
mpaka tuwe tumeshapita nchi yako."

18 [o]Lakini mfalme wa Edomu akajibu:

"Hamtapita hapa; kama mkijaribu
kupita, tutatoka na kuwashambulia
kwa upanga."

19 [p]Waisraeli wakajibu:

"Sisi tutafuata njia kuu; tena ikiwa
sisi au mifugo yetu tutakunywa tone la
maji yenu, tutalilipia. Sisi tunataka tu
kupita kwa miguu, wala si kitu kingine
chochote."

20 Watu wa Edomu wakajibu tena:

"Hamwezi kupita hapa."

Ndipo watu wa Edomu wakatoka dhidi ya
Waisraeli, jeshi kubwa lenye nguvu. 21 [q]Kwa
kuwa Waedomu waliwakatalia Waisraeli

[a]**20:4** Hes 14:2; Kut 14:11; Hes 14:3; 16:13
[b]**20:5** Hes 13:23; 16:14; Kut 17:1
[c]**20:6** Kut 40:2; Hes 14:5; 16:19
[d]**20:8** Kut 4:2; 10:12-13; 17:6; Isa 41:18; 43:20; Yer 31:9
[e]**20:9** Hes 17:2; 17:10
[f]**20:10** Za 106:32-33
[g]**20:11** Kut 17:6; Isa 33:21
[h]**20:12** Hes 27:14; Kum 32:51; Isa 5:16; 8:13; Kum 3:27
[i]**20:13** Kut 17:7; Law 10:3
[j]13 Meriba maana yake Kugombana.
[k]**20:14** Hes 20:1, 16; Mwa 36:16; 25:30; 24:3; Kum 4:39; Yos 2:11; 9:9; Kut 18:8
[l]**20:15** Mwa 46:6; 15:13; Kut 1:14
[m]**20:16** Mwa 16:11; 21:17; Kut 2:23; 14:19; 12:42; Kum 26:8; Hes 33:37
[n]**20:17** Hes 21:22; Kum 2:27; Amu 11:17
[o]**20:18** Hes 21:23
[p]**20:19** Kut 2:23; Kum 2:6, 28
[q]**20:21** Hes 21:23; 21:4; Kum 2:8; Amu 11:18

kupita katika nchi yao, Israeli wakageuka,
wakawaacha.

*Kifo Cha Aroni*

22 [a]Jumuiya yote ya Kiisraeli ikaondoka
kutoka Kadeshi, wakafika kwenye Mlima
Hori. 23 Kwenye Mlima Hori, karibu na
mpaka wa Edomu, BWANA akamwambia
Mose na Aroni, 24 [b]"Aroni atakusanywa
pamoja na watu wake. Hataingia katika
nchi ninayowapa Waisraeli, kwa sababu
ninyi wawili mliasi dhidi ya agizo langu
kwenye maji ya Meriba. 25 [c]Watwae Aroni
na Eleazari mwanawe, na uwapandishe
juu katika Mlima wa Hori. 26 [d]Mvue Aroni
mavazi yake, na umvike Eleazari mwanawe,
kwa maana Aroni atakusanywa pamoja na
watu wake; atakufa huko."

27 [e]Mose akafanya kama BWANA
alivyomwagiza: Wakapanda Mlima Hori
mbele ya macho ya jumuiya yote ya
Kiisraeli. 28 [f]Mose akamvua Aroni mavazi
yake na kumvika mwanawe Eleazari
mavazi hayo. Naye Aroni akafia pale
juu ya mlima. Kisha Mose na Eleazari
wakateremka kutoka mlimani. 29 Jumuiya
yote ilipofahamu kwamba Aroni amekufa,
jamaa yote ya Kiisraeli wakamwomboleza
kwa siku thelathini.

*Nchi Ya Aradi Yaangamizwa*

21 [g]Mfalme wa Kikanaani wa Aradi
aliyeishi huko Negebu aliposikia
kwamba Waisraeli walikuwa wanakuja
kwa njia ya Atharimu, aliwashambulia
Waisraeli na kuwateka baadhi yao. 2 [h]Ndipo
Israeli akaweka nadhiri hii kwa BWANA:
"Ikiwa utawatia watu hawa mikononi
mwetu, tutaiangamiza kabisa miji yao."
3 [i]BWANA akasikiliza ombi la Waisraeli,
naye akawapa ushindi juu ya Wakanaani.
Wakawaangamiza kabisa na miji yao; hivyo
mahali pale pakaitwa Horma.[j]

*Nyoka Wa Shaba*

4 [k]Waisraeli wakasafiri kutoka mlima Hori
kupitia njia inayoelekea Bahari ya Shamu,[l]
kuizunguka Edomu. Lakini watu wakakosa
uvumilivu njiani, 5 [m]wakamnung'unikia
Mungu na Mose, wakisema, "Kwa nini
umetupandisha kutoka Misri ili tufe
jangwani? Hakuna mkate! Hakuna maji!
Nasi tunachukia sana chakula hiki duni!"

6 [n]Ndipo BWANA akapeleka nyoka wenye
sumu katikati yao; wakawauma watu, nao
Waisraeli wengi wakafa. 7 [o]Watu wakamjia
Mose na kusema, "Tumetenda dhambi
wakati tuliponena dhidi ya BWANA na
dhidi yako. Mwombe BWANA ili atuondolee
hawa nyoka." Hivyo Mose akawaombea
hao watu.

8 [p]BWANA akamwambia Mose,
"Tengeneza nyoka wa shaba na umweke
juu ya mti; yeyote aliyeumwa na nyoka
anaweza kumtazama na akaishi tena."
9 [q]Kwa hiyo Mose akatengeneza nyoka
wa shaba na kumweka juu ya mti. Kisha
wakati mtu yeyote aliumwa na nyoka, naye
akamtazama yule nyoka wa shaba, aliishi.

*Safari Kwenda Moabu*

10 [r]Waisraeli waliendelea na safari
yao na wakapiga kambi huko Obothi.

---

[a]**20:22** Kum 1:46; Hes 33:37; 34:7; Kum 32:50
[b]**20:24** Mwa 25; 8; Kut 17:7
[c]**20:25** Hes 33:38
[d]**20:26** Kut 28:1-4; 40:13; Law 16:4; Hes 27:13; 31:2
[e]**20:27** Hes 33:38
[f]**20:28** Kut 29:29; Hes 33:38; Kum 10:6; 32:50; Mwa 27:41; Law 10:6; Kum 34:8
[g]**21:1** Hes 33:40; Yos 12:14; Mwa 12:9; Hes 13:17; Kum 1:7; Amu 1:9
[h]**21:2** Law 7:16; Kut 22:20; Kum 2:34; Yos 2:10; 8:26; Yer 25:9; 50:21
[i]**21:3** Mwa 10:18; Hes 14:45
[j]3 Horma maana yake Maangamizi.
[k]**21:4** Hes 20:22; 14:25; Kum 2:1; 11:4; Hes 20:21; Kum 2:8; Amu 11:18
[l]4 Yaani Bahari Nyekundu au Bahari ya Mafunjo (ona 14:25).
[m]**21:5** Za 78:19; Kut 14:11; Hes 11:20; 14:2, 3; 20:3; 11:5
[n]**21:6** Kum 8:15; 32:33; Ay 20:14; Za 58:4; 140:3; Yer 8:17; 1Kor 10:9
[o]**21:7** Za 78:34; Hos 5:15; Hes 14:40; Kut 8:8; 1Sam 7:8; Yer 27:18; 37:3; Mdo 8:24; Hes 11:2
[p]**21:8** Yn 3:14
[q]**21:9** 2Fal 18:4; Yn 3:14-15
[r]**21:10** Hes 33:43

11 [a]Kisha wakaondoka Obothi na kupiga
kambi huko Iye-Abarimu, katika jangwa
linalotazamana na Moabu kuelekea mawio
ya jua. 12 [b]Kutoka hapo waliendelea mbele
wakapiga kambi kwenye Bonde la Zeredi.
13 [c]Wakasafiri kutoka hapo na kupiga kambi
kando ya Mto Arnoni, ambao uko katika
jangwa lililoenea hadi nchi ya Waamori.
Arnoni ni mpaka wa Moabu, kati ya Moabu
na Waamori. 14 [d]Ndiyo sababu Kitabu cha
Vita vya BWANA kinasema:

"…Mji wa Wahebu nchini Seifa na
mabonde
ya Arnoni, 15 [e]na miteremko ya
mabonde
inayofika hadi mji wa Ari
na huelekea mpakani mwa
Moabu."

16 [f]Kutoka hapo waliendelea mbele hadi
kisima cha Beeri; kwenye kisima ambacho
BWANA alimwambia Mose, "Wakusanye
watu pamoja, nami nitawapa maji."
17 [g]Kisha Israeli akaimba wimbo huu:

"Bubujika, ee kisima!
Imba kuhusu maji,
18 kuhusu kisima ambacho kilichimbwa
na wakuu,
ambacho watu mashuhuri
walikifukua,
watu mashuhuri wakiwa na fimbo
za utawala na bakora."

Kisha wakatoka jangwani kwenda Matana,
19 kutoka Matana wakafika Nahalieli,
kutoka Nahalieli wakafika Bamothi, 20 [h]na
kutoka Bamothi wakafika kwenye bonde
lililoko Moabu, mahali ambapo kilele cha
Pisga kinatazamana na nyika.

*Kushindwa Kwa Sihoni Na Ogu*

**(Kumbukumbu 2:26–3:11)**

21 [i]Israeli akawatuma wajumbe
kumwambia Sihoni mfalme wa Waamori:

22 [j]"Uturuhusu tupite katika nchi
yako. Hatutageuka kando kwenda
katika mashamba au mashamba ya
mizabibu, ama kunywa maji kutoka
kisima chochote. Tutasafiri kwenye
njia kuu ya mfalme hata tutakapokuwa
tumekwisha kupita katika nchi yako."

23 [k]Lakini Sihoni hakumruhusu Israeli
apite katika nchi yake. Alilikutanisha jeshi
lake lote, wakaondoka kwenda jangwani ili
kupigana na Israeli. Alipofika huko Yahazi,
akapigana na Israeli. 24 [l]Hata hivyo, Israeli
alimshinda kwa upanga na kuiteka ardhi
yake kutoka Arnoni mpaka Yaboki, lakini ni
hadi kufikia nchi ya Waamoni tu, kwa sababu
mipaka yake ilikuwa imezungushwa ukuta.
25 [m]Israeli akaiteka miji yote ya Waamori na
kuikalia, pamoja na Heshboni na makazi
yote yanayoizunguka. 26 [n]Heshboni ulikuwa
mji wa Sihoni mfalme wa Waamori, ambaye
alikuwa amepigana dhidi ya mfalme wa
Moabu aliyetangulia na akawa amechukua
ardhi yake yote mpaka Arnoni.
27 Ndiyo sababu watunga mashairi
husema:

"Njoo Heshboni na ujengwe tena;
mji wa Sihoni na ufanywe upya.

---

[a]**21:11** Mwa 36:35; Hes 33:44; Kum 34:8; Yer 40:11
[b]**21:12** Kum 2:13, 14
[c]**21:13** Hes 22:36; Kum 2:24; Yos 12:1; Amu 11:13, 18; 2Fal 10:33; Isa 16:2; Yer 48:20; Mwa 10:16
[d]**21:14** 1Sam 17:47; 18:17; 25:28
[e]**21:15** Kum 2:9, 18; Isa 15:1
[f]**21:16** Hes 25:1; 33:49; Amu 9:21; Isa 15:8
[g]**21:17** Kut 15:1
[h]**21:20** Hes 23:14; Kum 3:17; 34:1; Yos 12:3; 13:20
[i]**21:21** Mwa 32:3; Hes 32:33; Kum 1:4; Yos 2:10; 12:2; 13:10; Amu 11:19-21; 1Fal 4:19; Neh 9:22; Za 135:11; 136:19; Yer 48:4; 48:45; Kut 23:23
[j]**21:22** Hes 20:17
[k]**21:23** Hes 20:21; Kum 2:32; Yos 13:18; 21:36; Amu 11:20; Isa 15:4; Yer 48:21, 34; Hes 20:18
[l]**21:24** Kum 2; 33; 3:3; 29:7; Za 135:10-11; Amo 2:9; Kum 3:4; Mwa 32:22; Hes 32:33; Amu 11:13, 22; Mwa 19:38; Kum 2:37; Yos 13:10
[m]**21:25** Hes 13:29; Amu 10:11; 11:26; Amo 2:10; Hes 32:3; Kum 1:4; 29:7; Yos 9:10; 12:2; Isa 15:4; 16:8; Yer 48:2
[n]**21:26** Kum 29:7; Za 135:11; Hes 13:29

28 [a]"Moto uliwaka kutoka Heshboni,
mwali wa moto kutoka mji wa
Sihoni.
Uliteketeza Ari ya Moabu,
raiya wa mahali pa Arnoni
palipoinuka.
29 [b]Ole wako, ee Moabu!
Umeharibiwa, enyi watu wa
Kemoshi!
Amewatoa wanawe kuwa wakimbizi,
na binti zake kama mateka
kwa Mfalme Sihoni wa Waamori.

30 [c]"Lakini tumewashinda;
Heshboni umeharibiwa hadi
Diboni.
Tumebomoa hadi kufikia Nofa,
ulioenea hadi Medeba."

31 [d]Kwa hiyo Israeli akaishi katika nchi
ya Waamori.
32 [e]Baada ya Mose kutuma wapelelezi
kwenda mji wa Yazeri, Waisraeli waliteka
viunga vya mji huo na kuwafukuza
Waamori waliokuwa wanaishi huko.
33 [f]Kisha wakageuka na kwenda katika njia
inayoelekea Bashani, naye Ogu mfalme wa
Bashani pamoja na jeshi lake lote wakatoka
kupigana nao huko Edrei.
34 [g]BWANA akamwambia Mose,
"Usimwogope Ogu, kwa sababu
nimeshamkabidhi mikononi mwako,
pamoja na jeshi lake lote na nchi yake.
Mtendee kama ulivyomtendea Sihoni
mfalme wa Waamori, ambaye alitawala
huko Heshboni."
35 [h]Kwa hiyo wakamuua, pamoja na
wanawe na jeshi lake lote, bila ya kumwacha
hata mtu mmoja hai. Nao wakaimiliki nchi
yake.

*Balaki Anamwita Balaamu*

22 [i]Kisha Waisraeli wakasafiri katika
tambarare za Moabu na kupiga kambi
kando ya Mto Yordani, ng'ambo ya Yeriko.
2 [j]Basi Balaki mwana wa Sipori,
aliona mambo yale yote ambayo Israeli
aliwatendea Waamori, 3 [k]Moabu aliogopa,
kwa kuwa walikuwepo watu wengi sana.
Hakika, Moabu alijawa na hofu kubwa kwa
sababu ya Waisraeli.
4 [l]Wamoabu wakawaambia wazee wa
Midiani, "Umati huu wa watu unakwenda
kuramba kila kitu kinachotuzunguka, kama
maksai arambavyo majani ya shambani."
Kwa hiyo Balaki mwana wa Sipori,
ambaye alikuwa mfalme wa Moabu wakati
huo, 5 [m]akatuma wajumbe kwenda kumwita
Balaamu mwana wa Beori, ambaye alikuwa
huko Pethori, karibu na Mto Frati, katika
nchi yake ya kuzaliwa. Balaki akasema:

"Taifa limekuja kutoka Misri, nao
wamefunika uso wa nchi, nao wametua
karibu nami. 6 [n]Sasa uje kuwalaani
watu hawa, kwa kuwa wana nguvu
sana kuniliko. Kisha huenda nikaweza
kuwashinda na kuwatoa nje ya nchi.
Kwa kuwa ninajua kwamba, wale
unaowabariki wanabarikiwa na wale
unaowalaani wanalaaniwa."

---

[a]**21:28** Yer 48:45; Hes 11:1; 22:41; Kum 12:2; Yos 13:17; Isa 15:2; Yer 1:5
[b]**21:29** Hes 24:17; 2Sam 8:2; 1Nya 18:2; Za 60:8; Isa 25:10; Yer 48:46; Amu 10:6; 11:24; Rum 1:15; 1Fal 11:7; 2Fal 23:13; Yer 48:7; Isa 15:5; 16:2
[c]**21:30** Hes 32:3; Yos 13:19; Neh 11:25; Isa 15:2; Yer 48:18; Yos 13:16; 1Nya 19:7
[d]**21:31** Hes 13:29
[e]**21:32** Yos 2:1; 6:22; 7:2; Amu 18:2; 2Sam 10:3; 1Nya 19:3; Hes 32:1; Yos 13:25; 2Sam 24:5; 1Nya 6:8; Isa 16:8; Yer 48; 32
[f]**21:33** Hes 32:33; Kum 3:3; 31:11; Yos 2:10; 12:4; 13:30; 1Fal 4:19; Neh 9:22; Za 135:11; 136:20; Kum 3:4; 32:14; Yos 9:10; 1Fal 4:13; Kum 1:4; 3:1; Yos 12:4; 13:12; 19:37
[g]**21:34** Kum 3:2
[h]**21:35** Hes 21:35; Yos 9:10; 22:1; Hes 22:11; 13:29; Yos 2:7; Hes 31:12; 33:48; Kum 32:49; Yos 2:1
[i]**22:1** Hes 22:11; 13:29; Yos 2:7; Hes 31:12; 33:48; Kum 32:49; Yos 2:1
[j]**22:2** Hes 23:1-3; Yos 24:9; Amu 11:25; Mik 6:5; Ufu 2:14
[k]**22:3** Kut 15:15
[l]**22:4** Mwa 19:37; 25:2; Hes 32:17; 18:29; Ay 5:25; Za 72:16
[m]**22:5** Hes 24:25; 31:8; Kum 23:4; Yos 13:22; Neh 13:2; Mik 6:5; 2Pet 2:15; Mwa 2:14; Kut 13:3
[n]**22:6** Hes 23:17; 24:9, 10

7 [a]Wazee wa Moabu na wa Midiani
wakaondoka, wakiwa wamechukua ada
ya uaguzi. Walipokwenda kwa Balaamu,
wakamweleza kile Balaki alikuwa amesema.
8 Balaamu akawaambia, “Mlale hapa
usiku huu, nami nitawaletea jibu lile
BWANA atakalonipa.” Kwa hiyo wakuu wa
Moabu wakakaa naye.
9 [b]Mungu akamjia Balaamu na kumuuliza,
“Watu gani hawa walio pamoja nawe?”
10 Balaamu akamwambia Mungu, “Balaki
mwana wa Sipori, mfalme wa Moabu,
alinipelekea ujumbe huu: 11 ‘Taifa ambalo
limekuja kutoka Misri limefunika uso
wa nchi. Sasa uje unilaanie hao watu.
Kisha huenda nitaweza kupigana nao na
kuwafukuza.’ ”
12 [c]Lakini BWANA akamwambia Balaamu,
“Usiende pamoja nao. Hupaswi kulaani
watu hao, kwa kuwa wamebarikiwa.”
13 Asubuhi iliyofuata Balaamu akaamka,
akawaambia wakuu wa Balaki, “Rudini
katika nchi yenu, kwa kuwa BWANA
amenikataza nisiende pamoja nanyi.”
14 Kwa hiyo wakuu wa Moabu wakarudi
kwa Balaki na kumwambia, “Balaamu
amekataa kuja pamoja nasi.”
15 Kisha Balaki akatuma wakuu wengine,
wengi zaidi na wanaoheshimiwa zaidi
kuliko wale wa kwanza. 16 Wakafika kwa
Balaamu na kumwambia:

“Balaki mwana wa Sipori amesema
hivi: Usiruhusu kitu chochote kikuzuie
kuja kwangu, 17 [d]kwa sababu nitakulipa
vizuri sana na kufanya lolote usemalo.
Njoo unilaanie watu hawa.”

18 [e]Lakini Balaamu akawajibu, “Hata
kama Balaki angenipa jumba lake la
kifalme likiwa limejazwa fedha na dhahabu,
singeweza kufanya kitu chochote kikubwa
au kidogo ili kutenda kitu nje ya agizo la
BWANA Mungu wangu. 19 Mlale hapa usiku
huu kama wale wengine walivyofanya,
nami nitatafuta ni nini kingine BWANA
atakachoniambia.”
20 [f]Usiku ule BWANA akamjia Balaamu
na kumwambia, “Kwa kuwa watu hawa
wamekuja kukuita wewe, nenda nao, lakini
ufanye tu lile nitakalokuambia.”

*Punda Wa Balaamu*

21 Balaamu akaamka asubuhi, akatandika
punda wake akaenda pamoja na wakuu wa
Moabu. 22 [g]Lakini Mungu alikasirika sana
alipokwenda, naye malaika wa BWANA
akasimama barabarani kumpinga. Balaamu
alikuwa amepanda punda wake, na
watumishi wake wawili walikuwa pamoja
naye. 23 [h]Wakati punda alipomwona malaika
wa BWANA akiwa amesimama barabarani
akiwa na upanga uliofutwa mkononi
mwake, punda akageukia upande kuelekea
shambani. Balaamu akampiga ili amrudishe
barabarani.
24 Ndipo malaika wa BWANA akasimama
katika njia nyembamba iliyo kati ya
mashamba mawili ya mizabibu, yakiwa na
kuta pande zote mbili. 25 Punda alipomwona
malaika wa BWANA, alijisukumiza karibu
na ukuta, na kugandamiza mguu wa
Balaamu ukutani. Ndipo Balaamu akampiga
tena punda.
26 Kisha malaika wa BWANA akaendelea
mbele na kusimama mahali pembamba
ambapo hapakuwepo nafasi ya kugeuka,
upande wa kulia wala wa kushoto. 27 [i]Punda
alipomwona malaika wa BWANA, alilala
chini Balaamu angali amempanda, naye
Balaamu akakasirika na kumpiga kwa
fimbo yake. 28 [j]Kisha BWANA akakifungua
kinywa cha punda, akamwambia Balaamu,
“Nimekutendea nini kinachokufanya
unipige mara hizi tatu?”
29 [k]Balaamu akamjibu punda,
“Umenifanya mjinga! Kama ningelikuwa

[a]**22:7** Mwa 30:27
[b]**22:9** Mwa 20:3; Hes 23:5; 24:4
[c]**22:12** Mwa 12:2
[d]**22:17** Hes 24:11
[e]**22:18** Hes 22:37; 23:12, 26; 24:13; 1Fal 22:14; 2Nya 18:13; Yer 42:4
[f]**22:20** Mwa 20:3; Hes 23:5; 24; 13; 2Nya 18:13
[g]**22:22** Kut 4:14; Mwa 16:7; Amu 13:3, 6, 13
[h]**22:23** Yos 5:13
[i]**22:27** Hes 11:1; Yak 1:19
[j]**22:28** 2Pet 2:16
[k]**22:29** Kum 25:4; Mit 12:10; 27:23-27; Mt 15:19

na upanga mkononi mwangu, ningelikuua
sasa hivi."
30 Punda akamwambia Balaamu, "Je,
mimi si punda wako mwenyewe, ambaye
umenipanda siku zote, hadi leo? Je,
nimekuwa na tabia ya kufanya hivi kwako?"
Akajibu, "Hapana."
31 [a]Kisha Bwana akafungua macho ya
Balaamu, naye akamwona malaika wa
Bwana amesimama barabarani akiwa
ameufuta upanga wake. Balaamu akainama,
akaanguka kifudifudi.
32 Malaika wa Bwana akamuuliza
Balaamu, "Kwa nini umempiga punda
wako mara tatu hizi? Nimekuja kukuzuia
kwa sababu njia yako imepotoka mbele
yangu. 33 Punda aliniona na kunikwepa
mara hizi tatu. Kama punda hangenikwepa,
hakika ningekuwa nimeshakuua sasa, lakini
ningemwacha punda hai."
34 [b]Balaamu akamwambia malaika wa
Bwana, "Nimetenda dhambi. Sikutambua
kuwa umesimama barabarani kunizuia. Basi
kama haikupendezi, nitarudi."
35 Malaika wa Bwana akamwambia
Balaamu, "Uende na watu hao, lakini useme
tu lile nikuambialo." Kwa hiyo Balaamu
akaenda na wale wakuu wa Balaki.
36 [c]Balaki aliposikia kuwa Balaamu
anakuja, akatoka kumlaki katika mji wa
Moabu, katika mpaka wa Arnoni, ukingoni
mwa nchi yake. 37 Balaki akamwambia
Balaamu, "Je, sikukupelekea jumbe za
haraka? Kwa nini hukuja kwangu? Hivi
kweli mimi siwezi kukulipa?"
38 [d]Balaamu akajibu, "Vema, sasa
nimekuja kwako. Lakini kwani nina uwezo
wa kusema tu chochote? Ni lazima niseme
tu kile ambacho Mungu ataweka kinywani
mwangu."
39 Kisha Balaamu alikwenda na Balaki
mpaka Kiriath-Husothi. 40 [e]Balaki akatoa
dhabihu ya ng'ombe na kondoo; baadhi
yake akampa Balaamu na wakuu waliokuwa
pamoja naye. 41 [f]Asubuhi iliyofuata Balaki
akamchukua Balaamu mpaka Bamoth-Baali,
na kutoka huko Balaamu akawaona baadhi
ya watu.

*Ujumbe Wa Kwanza Wa Balaamu*

23 [g]Balaamu akasema, "Nijengee hapa
madhabahu saba, mnitayarishie
mafahali saba na kondoo dume saba."
2 Balaki akafanya kama Balaamu
alivyosema; hao wawili kila mmoja wao
akatoa fahali mmoja na kondoo dume
mmoja juu ya kila madhabahu.
3 [h]Kisha Balaamu akamwambia Balaki,
"Kaa hapa kando ya sadaka yako wakati
mimi ninakwenda kando. Huenda
Bwana atakuja kukutana nami. Lolote
atakalonifunulia, nitakuambia." Basi
akaenda hata mahali peupe palipoinuka.
4 [i]Mungu akakutana naye, kisha Balaamu
akasema, "Nimekwisha kutengeneza
madhabahu saba, na juu ya kila madhabahu
nimetoa sadaka ya fahali mmoja na kondoo
dume mmoja."
5 [j]Bwana akaweka ujumbe katika kinywa
cha Balaamu na kusema, "Rudi kwa Balaki
umpe ujumbe huu."
6 [k]Basi Balaamu akarudi kwa Balaki,
akamkuta amesimama kando ya sadaka
yake akiwa na wakuu wote wa Moabu.
7 [l]Ndipo Balaamu akasema ujumbe wake:

"Balaki amenileta kutoka Aramu,
mfalme wa Moabu kutoka milima
ya mashariki.
Akasema, 'Njoo, unilaanie Yakobo;
njoo unishutumie Israeli.'

---

[a]**22:31** Mwa 21:19
[b]**22:34** Mwa 39:9; Hes 14:40; 1Sam 15:24; 2Sam 12:13; 24:10; Ay 33:27; Za 51:4
[c]**22:36** Hes 21:13
[d]**22:38** Hes 23:5
[e]**22:40** Hes 23:1; Eze 45:25
[f]**22:41** Hes 21:28; 23:13
[g]**23:1** Hes 22:40
[h]**23:3** Kum 18:18; Yer 1:9
[i]**23:4** Mwa 25:24-26; Kut 22:21; 23:9; Kum 10:19
[j]**23:5** Kut 4:12, 15; Isa 59:21; Hes 22:20; Mit 21:30; Isa 47:12
[k]**23:6** Law 20:24; 1Fal 8:53; Efe 2:14
[l]**23:7** Hes 22:5, 6; 24:3-21; Yos 24:9; 2Sam 23:1; 2Fal 5:1; Mwa 24:10; Neh 13:2; Law 15:16; Hes 5:2, 3; 1Kor 5:11, 13

8 [a]Nitawezaje kuwalaani,
hao ambao Mungu hajawalaani?
Nitawezaje kuwashutumu
hao ambao BWANA
hakuwashutumu?
9 [b]Kutoka vilele vya miamba
ninawaona,
kutoka mahali palipoinuka
ninawatazama.
Ninaliona taifa ambalo wanaishi
peke yao,
nao hawahesabiwi kama
mojawapo ya mataifa.
10 [c]Ni nani awezaye kuhesabu mavumbi
ya Yakobo,
au kuhesabu robo ya Israeli?
Mimi na nife kifo cha mtu mwenye
haki,
na mwisho wangu na uwe kama
wao!"

11 Balaki akamwambia Balaamu, "Ni nini ulichonitendea? Nimekuleta ulaani adui zangu, lakini wewe badala yake umewabariki!"

12 Balaamu akajibu, "Je, hainipasi kusema kile BWANA anachoweka katika kinywa changu?"

*Ujumbe Wa Pili Wa Balaamu*

13 Ndipo Balaki akamwambia, "Twende pamoja mahali pengine ambapo unaweza kuwaona; utawaona baadhi tu wala si wote.
Nawe kutoka huko, unilaanie hao."
14 [d]Basi akampeleka kwenye shamba la Sofimu, juu ya kilele cha Mlima Pisga. Pale akajenga madhabahu saba na kutoa sadaka ya fahali na kondoo dume mmoja juu ya kila madhabahu.

15 Balaamu akamwambia Balaki, "Kaa hapa kando ya sadaka yako wakati ninapokwenda kuonana na Mungu kule."

16 BWANA akakutana na Balaamu, akaweka ujumbe katika kinywa chake akasema, "Rudi kwa Balaki umpe ujumbe huu."

17 [e]Basi Balaamu akarudi kwa Balaki, akamkuta amesimama kando ya sadaka yake, akiwa na wakuu wa Moabu. Balaki akamuuliza, "Je, BWANA amesema nini?"

18 [f]Ndipo Balaamu akasema ujumbe wake:

"Balaki, inuka na usikilize,
nisikie mimi, wewe mwana wa
Sipori.
19 [g]Mungu si mtu, hata aseme uongo,
wala yeye si mwanadamu, hata
ajute.
Je, anasema, kisha asitende?
Je, anaahidi, asitimize?
20 Nimepokea agizo kubariki;
amebariki, nami siwezi
kubadilisha.

21 "Haijaonekana bahati mbaya katika
Yakobo,
wala taabu katika Israeli.
BWANA, Mungu wao yu pamoja nao,
nayo sauti kuu ya Mfalme imo
katikati yao.
22 Mungu aliwatoa kutoka Misri;
wao wana nguvu za nyati.
23 Hakuna uchawi dhidi ya Yakobo,
wala hakuna uaguzi dhidi ya
Israeli.
Sasa itasemwa kuhusu Yakobo
na Israeli, 'Tazama yale Mungu
aliyotenda!'
24 Taifa lainuka kama simba jike;
linajiinua kama simba
ambaye hatulii mpaka amalize
kurarua mawindo yake
na kunywa damu ya mawindo
yake."

25 Kisha Balaki akamwambia Balaamu, "Usiwalaani kabisa, wala usiwabariki kabisa!"

26 Balaamu akajibu, "Je, sikukuambia ni lazima nifanye lolote analosema BWANA?"

[a]**23:8** Hes 22:12; Isa 43:13; Yos 24:10; Neh 13:2
[b]**23:9** Hes 22:41; Kut 33:16; Kum 32:8
[c]**23:10** Mwa 13:16; Za 16:3; 116:15
[d]**23:14** Isa 1:10-11; Hos 12:11
[e]**23:17** 1Sam 3:17
[f]**23:18** Amu 3:20
[g]**23:19** 1Sam 15:29

*Ujumbe Wa Tatu Wa Balaamu*

27 Basi Balaki akamwambia Balaamu, “Njoo, nikupeleke mahali pengine. Huenda itampendeza Mungu kukuruhusu unilaanie hao watu kutoka mahali hapo.” 28 Balaki akamchukua Balaamu juu ya Mlima Peori, unaotazamana na nyika.

29 Balaamu akasema, “Nijengee hapa madhabahu saba, uandae mafahali saba na kondoo dume saba kwa ajili yangu.”
30 Balaki akafanya kama Balaamu alivyosema, kisha akatoa sadaka ya fahali mmoja na kondoo dume mmoja juu ya kila madhabahu.

24 [a]Basi Balaamu alipoona imempendeza
Bwana kubariki Israeli, hakuendelea tena kutafuta uchawi kama nyakati nyingine, bali aligeuza uso wake kuelekea
nyikani. 2 [b]Balaamu alipotazama nje na kuona Israeli amepiga kambi kabila kwa kabila, Roho wa Mungu akawa juu yake,
3 [c]naye akatoa ujumbe wake:

“Ujumbe wa Balaamu mwana wa Beori,
ujumbe wake yeye ambaye jicho lake linaona vizuri;
4 [d]ujumbe wake yeye ambaye husikia maneno ya Mungu,
ambaye huona maono kutoka kwa Mwenyezi,[e]
ambaye huanguka kifudifudi,
na ambaye macho yake yamefunguka:

5 [f]“Tazama jinsi yalivyo mazuri mahema yako, ee Yakobo,
maskani yako, ee Israeli!

6 [g]“Kama mabonde, yanaenea,
kama bustani kando ya mto,
kama miti ya udi iliyopandwa na Bwana,
kama mierezi kando ya maji.
7 [h]Maji yatatiririka kutoka ndoo zake;
mbegu yake itakuwa na maji tele.

“Mfalme wake atakuwa mkuu kuliko Mfalme Agagi;
ufalme wake utatukuka.

8 [i]“Mungu alimleta kutoka Misri;
yeye ana nguvu kama nyati.
Anayararua mataifa yaliyo adui zake,
na kuvunja mifupa yao vipande vipande;
huwachoma kwa mishale yake.
9 [j]Hujikunyata na kuvizia kama simba,
kama simba jike; nani anayethubutu kumwamsha?

“Abarikiwe kila akubarikiye,
na alaaniwe kila akulaaniye!”

10 [k]Ndipo hasira ya Balaki ikawaka dhidi ya Balaamu. Akapiga mikono yake pamoja, akamwambia Balaamu, “Nilikuita uje kuwalaani adui zangu, lakini umewabariki
mara hizi tatu. 11 [l]Sasa ondoka upesi uende nyumbani! Mimi nilisema nitakuzawadia vizuri sana, lakini Bwana amekuzuia usizawadiwe.”
12 [m]Balaamu akamwambia Balaki, “Je, hukumbuki jinsi nilivyowaambia wajumbe uliowatuma kwangu? Niliwaambia hivi,
13 [n]‘Hata ikiwa Balaki angenipa jumba lake la kifalme likiwa limejazwa fedha na dhahabu, nisingeweza kufanya kitu chochote kwa matakwa yangu, kikiwa kizuri au kibaya, kwenda kinyume na agizo la Bwana, nami imenipasa kusema tu kile

[a]**24:1** Hes 23:20, 23, 28
[b]**24:2** Hes 11:25; 1Sam 19:20; 2Nya 15:1; Mt 7:21-22; 1Kor 12:8-10
[c]**24:3** Hes 23:7
[d]**24:4** Hes 22:9; Mwa 15:1; 1Sam 19:24; Eze 1:28; Dan 8:18; 10:15; 2Kor 12:2
[e]4 Mwenyezi hapa ina maana ya Shaddai kwa Kiebrania (pia 24:16).
[f]**24:5** Yer 4:20; 30:18; Mal 2:12
[g]**24:6** Mwa 2:10; Za 1:3; 45:8; 104:16; Wim 4:14; Ay 29:19; Eze 31:5
[h]**24:7** Kut 17:8-16; Kum 28:1; 2Sam 5:12; 1Nya 14:2; Za 89:27; 145:11-13
[i]**24:8** Kut 15:6; Yer 50:17; 2Sam 18:14; Za 45:5
[j]**24:9** Kut 23:23; Hes 23:24; Mwa 12:2, 3; 27:29; Za 122:6
[k]**24:10** Kut 4:14; Ay 27:23; 34:37; Mao 2:15; Eze 21:14; 22:13; 25:6; Hes 22:6; 23:7-11, 18-24; Kum 23:5
[l]**24:11** Hes 22:17
[m]**24:12** Hes 22:18
[n]**24:13** Hes 22:18, 20

BWANA atakachosema'? 14 [a]Sasa ninarudi
kwa watu wangu. Lakini njoo, nikuonye
kuhusu kile watu hawa watakachowatenda
watu wako siku zijazo."

*Ujumbe Wa Nne Wa Balaamu*

15 Kisha Balaamu akatoa ujumbe wake:

"Ujumbe wa Balaamu mwana wa
Beori,
ujumbe wake yeye ambaye jicho
lake linaona vizuri;
16 [b]ujumbe wake yeye ambaye husikia
maneno ya Mungu,
ambaye ana maarifa kutoka kwa
Aliye Juu Sana,
huona maono kutoka Mwenyezi,
ambaye huanguka kifudifudi
na ambaye macho yake
yamefunguka:

17 [c]"Namwona yeye, lakini si sasa;
namtazama yeye, lakini si karibu.
Nyota itatoka kwa Yakobo,
fimbo ya ufalme itainuka kutoka
kwa Israeli.
Atawaponda Wamoabu vipaji vya
nyuso
na mafuvu yote ya wana wa
Shethi.
18 [d]Edomu itamilikiwa,
Seiri, adui wake, itamilikiwa,
lakini Israeli atakuwa na nguvu.
19 [e]Mtawala atakuja kutoka kwa Yakobo
na kuangamiza walionusurika
katika mji."

*Ujumbe Wa Mwisho Wa Balaamu*

20 [f]Kisha Balaamu akawaona watu wa
Amaleki, na kutoa ujumbe wake:

"Amaleki ilikuwa ya kwanza
miongoni mwa mataifa,
lakini mwisho wake itaangamizwa
milele."

21 [g]Kisha akawaona Wakeni, akatoa
ujumbe wake:

"Makao yenu ni salama,
kiota chenu kiko kwenye
mwamba.
22 [h]Hata hivyo ninyi Wakeni
mtaangamizwa
Ashuru atakapowachukua
mateka."

23 Ndipo akatoa ujumbe wake:

"Lo, ni nani atakayeweza kuishi
wakati Mungu atakapofanya
hili?
24 [i]Meli zitakuja kutoka pwani za
Kitimu,
zitaitiisha Ashuru na Eberi,
lakini nao pia wataangamizwa."

25 Kisha Balaamu akainuka na kurudi
nyumbani kwake, naye Balaki akashika
njia yake.

*Moabu Yashawishi Israeli*

25 [j]Israeli alipokuwa akikaa Shitimu,
wanaume wa Israeli walianza kuzini
na wanawake wa Kimoabu, 2 [k]ambao
waliwaalika kushiriki katika kutoa kafara
kwa miungu yao. Watu wakala na kusujudu
mbele ya miungu hii. 3 [l]Kwa hiyo Israeli
akaungana katika kumwabudu Baali wa
Peori. Hasira ya BWANA ikawaka dhidi yao.

[a]**24:14** Mwa 49:1; Hes 31:8; Mik 6:5
[b]**24:16** Hes 22:9; Mwa 14:18; Isa 14:14
[c]**24:17** Ufu 1:7; Mt 2:2; Mwa 49:10; 19:37; Hes 21:29; Kum 23:6; Isa 15:1–16:14; Yer 48:45
[d]**24:18** 2Sam 8:12; 1Nya 18:11; Za 60:8; Isa 11:14; Amo 9:12; Mwa 9:25; 14:6; Kum 1:44; Yos 12:7; 15:10; Amu 5:4; Oba 1:2
[e]**24:19** Mwa 49:10; Mik 5:2
[f]**24:20** Mwa 14:7; Kut 17:14; Kum 25:19; 1Sam 15:20; 30:17-20; 2Sam 8:12; 1Nya 18:11
[g]**24:21** Mwa 15:19; Za 37:27; Mit 1:33; Isa 32:18; Eze 34:27
[h]**24:22** Mwa 10:22
[i]**24:24** Mwa 10:4, 21; Hes 22:5; Isa 23:1; Dan 11:30; Law 26:28; Kum 28:36; Mt 23:37
[j]**25:1** Hes 21:16; Yos 2:1; Isa 66:11; Yoe 3:18; Mik 6:5; Yer 5:7; 7:9; 9:2; 1Kor 10:8; Ufu 2:14; Mwa 19:37; Hes 31:16
[k]**25:2** Kut 32:6; 20:5; Kum 32:38; 1Kor 10:20; Yos 22:17; Hos 9:10; Kut 34:15; 20:5
[l]**25:3** Kum 4:19; Amu 2:19; 1Fal 9:9; Yer 1:16; 44:3; Hes 23:26

4 [a]Bwana akamwambia Mose,
“Uwachukue viongozi wote wa watu hawa,
uwaue na uwaweke hadharani mchana
peupe mbele za Bwana, ili hasira kali ya
Bwana iweze kuondoka kwa Israeli.”
5 [b]Kwa hiyo Mose akawaambia waamuzi
wa Israeli, “Kila mmoja wenu lazima awaue
wale wanaume wenu, walioshiriki katika
kumwabudu Baali wa Peori.”
6 [c]Ndipo mwanaume wa Kiisraeli akamleta
mwanamke wa Kimidiani katika jamaa yake
palepale mbele ya Mose na mkutano wote
wa Israeli walipokuwa wakilia kwenye lango
la Hema la Kukutania. 7 [d]Finehasi mwana wa
Eleazari, mwana wa kuhani Aroni, alipoona
jambo hili, akaondoka kwenye kusanyiko,
akachukua mkuki mkononi mwake,
8 [e]akamfuata yule Mwisraeli ndani ya hema.
Akawachoma mkuki wote wawili kwa
pamoja, ukapenya kwenye mwili wa yule
Mwisraeli na mwili wa yule mwanamke.
Ndipo tauni iliyokuwepo dhidi ya Waisraeli
ikakoma. 9 [f]Lakini wale waliokufa kwa hiyo
tauni walikuwa watu 24,000.
10 Bwana akamwambia Mose,
11 [g]“Finehasi mwana wa Eleazari, mwana
wa kuhani Aroni, amegeuza hasira yangu
mbali na Waisraeli, kwa sababu alikuwa na
wivu kama nilio nao kwa heshima yangu
miongoni mwao, hata kwamba kwa wivu
wangu sikuwaangamiza. 12 [h]Kwa hiyo
mwambie Finehasi ninafanya Agano langu
la amani naye. 13 [i]Yeye pamoja na wazao
wake watakuwa na Agano la ukuhani
milele, kwa sababu alikuwa na wivu
kwa ajili ya heshima ya Mungu wake, na
akafanya upatanisho kwa Waisraeli.”
14 [j]Jina la Mwisraeli ambaye aliuawa
pamoja na mwanamke wa Kimidiani ni
Zimri mwana wa Salu, kiongozi wa jamaa
ya Simeoni. 15 [k]Jina la mwanamke wa
Kimidiani aliyeuawa ni Kozbi binti wa
Suri, aliyekuwa mkuu wa kabila la jamaa
ya Wamidiani.
16 [l]Bwana akamwambia Mose,
17 [m]“Watendeeni Wamidiani kama adui na
mwaue, 18 [n]kwa sababu wao waliwatendea
kama adui wakati waliwadanganya katika
tukio la Peori na dada yao Kozbi, binti wa
kiongozi wa Kimidiani, mwanamke ambaye
aliuawa wakati tauni ilikuja kama matokeo
ya tukio la Peori.”

### *Kuhesabiwa Watu Mara Ya Pili*

26 [o]Baada ya hiyo tauni, Bwana
akamwambia Mose na Eleazari mwana
wa kuhani Aroni, 2 [p]“Hesabu jumuiya yote
ya Kiisraeli kwa jamaa zao, wale wote
wenye umri wa miaka ishirini na zaidi,
ambao wanaweza kutumika katika jeshi
la Israeli.” 3 [q]Hivyo Mose na kuhani Eleazari
wakazungumza na watu kwenye nchi
tambarare ya Moabu, ng’ambo ya Yordani
kutokea Yeriko, wakasema, 4 [r]“Hesabuni
wanaume wenye umri wa miaka ishirini na
zaidi, kama Bwana alivyomwagiza Mose.”

Hawa ndio Waisraeli waliotoka Misri:

5 [s]Wazao wa Reubeni, mwana mzaliwa wa
kwanza wa Israeli, walikuwa:

---

[a]**25:4** Hes 7:2; 13:3; 2Sam 21:6; Kum 4:3; Kut 32:12; Kum 13:17; Yos 7:26; 2Fal 23:26; 2Nya 28:11; 29:10; 30:8; Eze 10:14; Yer 44:3
[b]**25:5** Kut 32:27; Hos 9:10
[c]**25:6** Mwa 25:2; Hes 14:1; Amu 2:4; Rut 1:9; 1Sam 11:4; 2Sam 15:30; Ezr 10:1; Za 126:6; Yer 41:6
[d]**25:7** Kut 6:25; Yos 22:13; Amu 20:28; 5:8; 1Sam 13:19; 1Fal 18:28; Za 35:3; 46:9; Yoe 3:10; Mik 4:3
[e]**25:8** Za 106:30
[f]**25:9** Hes 14:37; 1Kor 10:8; Hes 31:16
[g]**25:11** Za 106:30; Kut 20:5; Kum 32:16; Za 78:58; Nah 1:3; Sef 1:13
[h]**25:12** Isa 11:9; 54:10; Eze 34:25; 37:26; Mal 2:4
[i]**25:13** Kut 29:9; 1Fal 19:10; 2Fal 10:16; Kut 29:36; Rum 3:26; Za 106:31; Yer 33:18
[j]**25:14** Hes 1:6; 25:6
[k]**25:15** Hes 31:8; Yos 13:21; Hab 3:7
[l]**25:16** Hes 31:7
[m]**25:17** Hes 31:1-3; Kut 23:22; Amu 2:16-18; Neh 9:27; Za 8:2; 21:8; 74:23; Kum 21:1; 1Sam 17:9; 2Fal 9:27; 10:25
[n]**25:18** Hes 23:28
[o]**26:1** Hes 14:37; 25:8
[p]**26:2** Kut 30:11-16; Hes 1:3; Kut 38:25
[q]**26:3** Hes 33:48; Yos 13:22; Hes 22:1; Kum 4:46-49
[r]**26:4** Kut 6:14; 13:3
[s]**26:5** Hes 1:20; Mwa 46:8, 9; 1Nya 5:3; Ufu 7:5

kutoka kwa Hanoki, ukoo wa Wahanoki;
kutoka kwa Palu, ukoo wa Wapalu;
6 [a]kutoka kwa Hesroni, ukoo wa Wahesroni;
kutoka kwa Karmi, ukoo wa Wakarmi.

7 Hizi zilikuwa ndizo koo za Reubeni; wale
waliohesabiwa walikuwa 43,730.
8 Mwana wa Palu alikuwa Eliabu, 9 [b]nao
wana wa Eliabu walikuwa Nemueli,
Dathani na Abiramu. Hawa wawili Dathani
na Abiramu ndio walikuwa maafisa wa
jumuiya ambao walimwasi Mose na Aroni,
na walikuwa miongoni mwa wafuasi wa
Kora wakati walimwasi BWANA. 10 [c]Ardhi
ilifunua kinywa chake na kuwameza
pamoja na Kora, ambaye wafuasi wake
walikufa wakati moto ulipowateketeza
wanaume 250. Nao walikuwa kama alama
ya onyo. 11 [d]Pamoja na hayo, hao ukoo wa
Kora hawakufa.

12 [e]Wazao wa Simeoni kwa koo zao walikuwa:

kutoka kwa Nemueli, ukoo wa Wanemueli;
kutoka kwa Yamini, ukoo wa Wayamini;
kutoka wa Yakini, ukoo wa Wayakini;
13 [f]kutoka kwa Zera, ukoo wa Wazera;
kutoka kwa Shauli, ukoo wa Washauli.

14 [g]Hizi ndizo koo za Simeoni; walikuwa 22,200.

15 [h]Wazao wa Gadi kwa koo zao walikuwa:

kutoka kwa Sifoni, ukoo wa Wasifoni;
kutoka kwa Hagi, ukoo wa Wahagi;
kutoka kwa Shuni, ukoo wa Washuni;
16 kutoka kwa Ozni, ukoo wa Waozni;
kutoka kwa Eri, ukoo wa Waeri;
17 [i]kutoka kwa Arodi, ukoo wa Waarodi;
kutoka kwa Areli, ukoo wa Waareli.

18 [j]Hizi ndizo zilizokuwa koo za Gadi; wale waliohesabiwa walikuwa 40,500.

19 [k]Eri na Onani walikuwa wana wa Yuda, lakini walifia huko Kanaani.
20 [l]Wazao wa Yuda kwa koo zao walikuwa:

kutoka kwa Shela, ukoo wa Washela;
kutoka kwa Peresi, ukoo wa Waperesi;
kutoka kwa Zera, ukoo wa Wazera.
21 [m]Wazao wa Peresi walikuwa:
kutoka kwa Hesroni, ukoo wa Wahesroni;
kutoka kwa Hamuli, ukoo wa Wahamuli.

22 [n]Hizi ndizo zilizokuwa koo za Yuda; wale waliohesabiwa walikuwa 76,500.

23 [o]Wazao wa Isakari kwa koo zao walikuwa:

kutoka kwa Tola, ukoo wa Watola;
kutoka kwa Puva, ukoo wa Wapuva;
24 [p]kutoka kwa Yashubu, ukoo wa Wayashubu;
kutoka kwa Shimroni, ukoo wa Washimroni.

25 [q]Hizi ndizo zilizokuwa koo za Isakari; wale waliohesabiwa walikuwa 64,300.

26 [r]Wazao wa Zabuloni kwa koo zao walikuwa:

---

[a]**26:6** 1Nya 5:3; Mwa 46:9
[b]**26:9** Hes 16:1; 1:16; 16:2; Isa 65:16; Kum 11:6; Hes 27:3; 16:1, 2
[c]**26:10** Kut 15:12; Hes 16:35, 38; Kut 3:12; Ay 31:3; Za 145:20; Yer 29:22; 2Pet 2:6; Yud 7
[d]**26:11** Kut 6:24; Hes 16:33; Kum 5:9; 24:16; 2Fal 14:6; 2Nya 25:4; Eze 18:20
[e]**26:12** Mwa 46:10; 1Nya 4:24; Kut 6:15
[f]**26:13** Mwa 46:10
[g]**26:14** Mwa 46:10; Hes 1:23
[h]**26:15** Mwa 46:16
[i]**26:17** Mwa 46:16
[j]**26:18** Mwa 30:11; Hes 1:25; Yos 13:24-28
[k]**26:19** Mwa 38:3; 38:4; 38:7; 46:12; 1Nya 2:3
[l]**26:20** Mwa 38:5; 38:29; Yos 7:17
[m]**26:21** Mwa 38:29; Rut 4:19; 1Fal 2:9
[n]**26:22** Hes 1:27
[o]**26:23** Mwa 46:13; 49:14
[p]**26:24** Mwa 46:13
[q]**26:25** Mwa 30:18
[r]**26:26** Hes 1:30; Mwa 46:14; 49:13

kutoka kwa Seredi, ukoo wa Waseredi;
kutoka kwa Eloni, ukoo wa Waeloni;
kutoka kwa Yaleeli, ukoo wa Wayaleeli.

27 [a]Hizi ndizo zilizokuwa koo za Zabuloni, wale waliohesabiwa walikuwa 60,500.

28 [b]Wazao wa Yosefu kwa koo zao kutoka kwa Manase na kwa Efraimu walikuwa:

29 [c]Wazao wa Manase:

kutoka kwa Makiri, ukoo wa Wamakiri (Makiri alikuwa baba wa Gileadi);
kutoka kwa Gileadi, ukoo wa Wagileadi.
30 [d]Hawa ndio waliokuwa wazao wa Gileadi:
kutoka kwa Iezeri, ukoo wa Waiezeri;
kutoka kwa Heleki, ukoo wa Waheleki;
31 kutoka kwa Asirieli, ukoo wa Waasirieli;
kutoka kwa Shekemu, ukoo wa Washekemu;
32 kutoka kwa Shemida, ukoo wa Washemida;
kutoka kwa Heferi, ukoo wa Waheferi.
33 [e](Selofehadi mwana wa Heferi hakuzaa wana, bali alikuwa na watoto wa kike tu, ambao majina yao yalikuwa Mahla, Noa, Hogla, Milka na Tirsa.)

34 [f]Hizi ndizo zilizokuwa koo za Manase; wale waliohesabiwa walikuwa 52,700.

35 [g]Hawa walikuwa wazao wa Efraimu kwa koo zao:

kutoka kwa Shuthela, ukoo wa Washuthela;
kutoka kwa Bekeri, ukoo wa Wabekeri;
kutoka kwa Tahani, ukoo wa Watahani;
36 Hawa ndio walikuwa wazao wa Shuthela:
kutoka kwa Erani, ukoo wa Waerani.

37 [h]Hizi ndizo zilizokuwa koo za Efraimu; wale waliohesabiwa walikuwa 32,500.

Hawa ndio waliokuwa wazao wa Yosefu kwa koo zao.

38 [i]Wazao wa Benyamini kwa koo zao walikuwa:

kutoka kwa Bela, ukoo wa Wabela;
kutoka kwa Ashbeli, ukoo wa Waashbeli;
kutoka kwa Ahiramu, ukoo wa Waahiramu;
39 [j]kutoka kwa Shufamu, ukoo wa Washufamu;
kutoka kwa Hufamu, ukoo wa Wahufamu.
40 [k]Wazao wa Bela kutoka kwa Ardi na Naamani walikuwa:
kutoka kwa Ardi, ukoo wa Waardi;
kutoka kwa Naamani, ukoo wa Wanaamani.

41 [l]Hizi ndizo zilizokuwa koo za Benyamini; wale waliohesabiwa walikuwa 45,600.

42 [m]Hawa ndio waliokuwa wazao wa Dani kwa koo zao:

kutoka kwa Shuhamu, ukoo wa Washuhamu.

---

[a]**26:27** Mwa 30:20
[b]**26:28** Hes 1:32; 36:1; Mwa 41:52; 46:20; 48:3
[c]**26:29** Hes 1:34; Mwa 50:23; Amu 11:1; Hes 32:39
[d]**26:30** Hes 27:1; 36:1; 1Nya 7:14; Yos 17:2; Amu 6:11; 8:2
[e]**26:33** Hes 27:1; 36:2; Yos 17:3; 1Nya 7:15; Hes 27:3; 36:11
[f]**26:34** Hes 1:35
[g]**26:35** Hes 1:32; 1Nya 7:20
[h]**26:37** Hes 1:33; Kum 33:13-17
[i]**26:38** Mwa 46:21; Hes 1:36; 1Nya 8:40
[j]**26:39** Mwa 46:21; 1Nya 7:12
[k]**26:40** Mwa 46:21; 1Nya 8:3
[l]**26:41** Hes 1:37
[m]**26:42** Hes 1:38, 39; Amu 18:19; Mwa 46:23; 49:16; Kum 33:22

Hizi ndizo zilizokuwa koo za Dani: 43 Wote
walikuwa koo za Washuhamu; wale
waliohesabiwa walikuwa 64,400.

44 [a]Wazao wa Asheri kwa koo zao walikuwa:

kutoka kwa Imna, ukoo wa Waimna;
kutoka kwa Ishvi, ukoo wa Waishvi;
kutoka kwa Beria, ukoo wa Waberia;
45 kutoka kwa wazao wa Beria:
kutoka kwa Heberi, ukoo wa Waheberi;
kutoka kwa Malkieli, ukoo wa Wamalkieli.
46 (Asheri alikuwa na binti aliyeitwa Sera.)

47 Hizi ndizo zilizokuwa koo za Asheri; wale
waliohesabiwa walikuwa 53,400.

48 [b]Wazao wa Naftali kwa koo zao walikuwa:

kutoka kwa Yaseeli, ukoo wa Wayaseeli;
kutoka kwa Guni, ukoo wa Waguni;
49 [c]kutoka kwa Yeseri, ukoo wa Wayeseri;
kutoka kwa Shilemu, ukoo wa Washilemu.

50 [d]Hizi ndizo zilizokuwa koo za Naftali;
wale waliohesabiwa walikuwa 45,400.

51 [e]Jumla ya hesabu ya wanaume wa Israeli
ilikuwa 601,730.

52 BWANA akamwambia Mose,
53 [f]"Watagawiwa nchi kama urithi kwa
kulingana na hesabu ya majina. 54 [g]Kundi
kubwa zaidi lipe urithi mkubwa zaidi, na
kundi dogo zaidi lipewe urithi mdogo zaidi;
kila kundi litapokea urithi wake kulingana
na hesabu ya wale walioorodheshwa.
55 [h]Hakikisha kuwa nchi inagawanywa kwa
kura. Kile kitakachorithiwa na kila kikundi
kitakuwa kwa kulingana na majina ya kabila
la babu yao. 56 Kila urithi utagawanywa kwa
kura miongoni mwa makundi makubwa na
madogo."

57 [i]Hawa walikuwa Walawi ambao
walihesabiwa kwa koo zao:

kutoka kwa Gershoni, ukoo wa Wagershoni;
kutoka kwa Kohathi, ukoo wa Wakohathi;
kutoka kwa Merari, ukoo wa Wamerari.
58 [j]Hizi pia zilikuwa koo za Walawi:
ukoo wa Walibni;
ukoo wa Wahebroni;
ukoo wa Wamahli;
ukoo wa Wamushi;
ukoo wa wana wa Kora.
(Kohathi alikuwa baba aliyemzaa
Amramu; 59 [k]jina la mke wa Amramu
ni Yokebedi, naye pia alikuwa
mzao wa Lawi, ambaye alizaliwa
kwa Walawi nchini Misri. Alimzalia
Amramu: Aroni, Mose na dada yao
Miriamu. 60 [l]Aroni alikuwa baba
yake Nadabu na Abihu, Eleazari
na Ithamari. 61 [m]Lakini Nadabu na
Abihu walikufa wakati walitoa
sadaka mbele za BWANA kwa moto
usioruhusiwa.)

62 [n]Wanaume wote wa Walawi wa umri wa
mwezi mmoja na zaidi walikuwa 23,000.
Wao hawakuhesabiwa pamoja na Waisraeli
wengine kwa sababu hawakupokea urithi
miongoni mwao.

63 [o]Hawa ndio walioorodheshwa na Mose
na kuhani Eleazari wakati waliwahesabu
Waisraeli kwenye nchi tambarare ya Moabu,
kando ya Yordani ng'ambo ya Yeriko.
64 [p]Hakuna hata mmoja wao aliyekuwa
miongoni mwa wale waliohesabiwa na
Mose na kuhani Aroni wakati waliwahesabu

[a]**26:44** Hes 1:40; 26:47; 1:41
[b]**26:48** Mwa 30:8; 46:24; 1Nya 7:13
[c]**26:49** 1Nya 7:13
[d]**26:50** Hes 1:42, 43
[e]**26:51** Kut 12:37; Hes 1:46; 2:32
[f]**26:53** Yos 11:23; 14:1; Eze 45:8
[g]**26:54** Hes 33:54; 35:8
[h]**26:55** Hes 34:13; Yos 11:23; 14:2
[i]**26:57** Mwa 46:11; Kut 6:16; 1Nya 6:16
[j]**26:58** Kut 6:20
[k]**26:59** Kut 2:1; 6:20; 2:4; 15:20
[l]**26:60** Kut 6:23
[m]**26:61** Law 10:1-2; Hes 3:4; 1Nya 24; 2
[n]**26:62** Hes 3:39; 1:47; 18:23; 2:33; 18:20-24; 35:2-8; Kum 14:27-29
[o]**26:63** Hes 1:19; 22:1
[p]**26:64** Hes 14:29; 1:44; 1:1; Kum 2:14, 15

Waisraeli katika Jangwa la Sinai. 65 [a]Kwa
maana BWANA alikuwa amewaambia hao
Waisraeli hakika wangekufa huko jangwani,
wala hakuna mmoja wao aliyeachwa,
isipokuwa Kalebu mwana wa Yefune na
Yoshua mwana wa Nuni.

*Binti Wa Selofehadi*

27 [b]Binti za Selofehadi mwana wa Heferi,
mwana wa Gileadi, mwana wa Makiri,
mwana wa Manase, walikuwa wa koo za
Manase mwana wa Yosefu. Majina ya hao
binti yalikuwa Mahla, Noa, Hogla, Milka
na Tirsa. Walikaribia 2 [c]ingilio la Hema la
Kukutania na kusimama mbele ya Mose,
kuhani Eleazari, viongozi na kusanyiko lote,
wakasema, 3 [d]"Baba yetu alikufa jangwani.
Hakuwa miongoni mwa wafuasi wa Kora,
ambao walifungamana pamoja dhidi ya
BWANA, lakini alikufa kwa ajili ya dhambi
yake mwenyewe na hakuacha wana. 4 Kwa
nini jina la baba yetu lifutike kutoka ukoo
wake kwa sababu hakuwa na mwana?
Tupatie milki miongoni mwa ndugu za
baba yetu."

5 [e]Kwa hiyo Mose akalileta shauri
lao mbele za BWANA, 6 naye BWANA
akamwambia Mose, 7 [f]"Wanachosema binti
za Selofehadi ni sawa. Ni lazima kwa hakika
uwape milki kama urithi miongoni mwa
ndugu za baba yao, na kubadili urithi wa
baba yao uwe wao.

8 "Waambie Waisraeli, 'Ikiwa mtu atakufa
naye hakuacha mwana, utampa binti yake
urithi wake. 9 Ikiwa hana binti, wape ndugu
zake wa kiume urithi wake. 10 Ikiwa hana
ndugu wa kiume toa urithi wake kwa ndugu
za baba yake. 11 [g]Ikiwa baba yake hakuwa
na ndugu wa kiume, toa urithi wake kwa
ndugu wa karibu katika ukoo wake, ili
aumiliki. Hili litakuwa dai la sheria kwa
Waisraeli, kama BWANA alivyomwamuru
Mose.' "

*Yoshua Kuchukua Nafasi Ya Mose*

**(Kumbukumbu 31:1-8)**

12 [h]Kisha BWANA akamwambia Mose,
"Panda juu ya mlima huu katika kilele
cha Abarimu uione nchi ambayo nimewapa
Waisraeli. 13 [i]Baada ya kuiona, wewe pia
utakusanywa pamoja na watu wako kama
ndugu yako Aroni alivyokusanywa, 14 [j]kwa
kuwa jumuiya ilipoasi amri yangu kwenye
maji katika Jangwa la Sini, wakati jumuiya
ilipogombana nami, nyote wawili mliacha
kuitii amri yangu ya kuniheshimu kama
mtakatifu mbele ya macho yao." (Haya
yalikuwa maji ya Meriba huko Kadeshi,
katika Jangwa la Sini.)

15 Mose akamwambia BWANA,
16 [k]"BWANA, Mungu wa roho zote za
wanadamu, na amteue mtu juu ya jumuiya
hii 17 [l]ili atoke na kuingia mbele yao,
atakayewaongoza katika kutoka kwao na
kuingia kwao, ili watu wa BWANA wasiwe
kama kondoo wasio na mchungaji."

18 [m]Kwa hiyo BWANA akamwambia Mose,
"Mchukue Yoshua mwana wa Nuni, mtu
ambaye Roho yuko ndani yake, uweke
mkono juu yake. 19 [n]Msimamishe mbele
ya kuhani Eleazari pamoja na kusanyiko
lote, umpe maagizo mbele yao. 20 [o]Mpe
sehemu ya mamlaka yako ili jumuiya yote

[a]**26:65** Hes 14:18; 1Kor 10:5; Hes 13:6; 11:28; Za 90:3-8; Rum 11:22; Kum 32:49-50; Yos 14:10; Hes 14:18, 30; Ebr 3:17, 18; Yud 5
[b]**27:1** Hes 26:33; Yos 17:2, 3; Hes 26:30; Mwa 50:23; 1Nya 2:21
[c]**27:2** Kut 40:2; Hes 9:6; 1:16; 31:13; 32:2; 36:1
[d]**27:3** Hes 26:65; 16:2; 26:33
[e]**27:5** Mwa 25:22; Kut 18:19; Hes 9:8; Kut 25:22; Law 24:12-13; Mit 3:5-6
[f]**27:7** Ay 42:15; 17:4; Hes 36:2
[g]**27:11** Hes 35:29
[h]**27:12** Hes 23:14; 33:47; Yer 22:20; Kum 3:23; 32:48-52; Law 14:34
[i]**27:13** Hes 20:12; 31:2; Kum 4:22; 31:14; 32:50; 1Fal 2:1; Hes 20:28
[j]**27:14** Hes 20:1; 20:12; Kut 17:7; Kum 1:37; 32:51; Za 106:32
[k]**27:16** Hes 16:22; Ay 21:10; Ebr 12:9; Zek 12:1
[l]**27:17** 1Fal 22:17; 2Nya 18:16; Eze 34:5; Zek 10:2; Mt 9:36; Kum 31:2; 1Sam 8:20; 18:13; 2Nya 1:10; 18:16; Amu 3:10
[m]**27:18** Mwa 41:38; Hes 11:25; Kum 34:9; Mdo 6:6; Amu 3:10
[n]**27:19** Kum 3:28; 31:14; 31:7
[o]**27:20** Ay 1:16; Hes 11:17; 1Sam 10:6; 2Fal 2:15

ya Waisraeli ipate kumtii. 21 [a]Atasimama
mbele ya kuhani Eleazari, ambaye atapokea
maamuzi kwa ajili yake, kwa kuuliza mbele
za BWANA kwa ile Urimu.[b] Kwa amri
yake, yeye na jumuiya yote ya Waisraeli
watatoka, na kwa amri yake, wataingia."
22 Mose akafanya kama BWANA
alivyomwagiza. Akamtwaa Yoshua na
kumsimamisha mbele ya kuhani Eleazari na
kusanyiko lote. 23 [c]Kisha akaweka mikono
yake juu ya kichwa cha Yoshua na kumpa
maagizo, kama vile BWANA alivyoelekeza
kupitia kwa Mose.

*Sadaka Za Kila Siku*

**(Kutoka 29:38-46)**

28 BWANA akamwambia Mose, 2 [d]"Wape
Waisraeli agizo hili na uwaambie:
'Hakikisheni kwamba mnaniletea mimi
kwa wakati uliowekwa chakula kwa ajili
ya sadaka za kuteketezwa kwa moto, kama
harufu nzuri ya kupendeza.' 3 [e]Waambie:
'Hii ni sadaka ya kuteketezwa kwa moto
mnayomtolea BWANA: wana-kondoo wawili
wa mwaka mmoja wasio na dosari, kama
sadaka ya kawaida ya kuteketezwa kila siku.
4 [f]Andaa mwana-kondoo mmoja asubuhi
na mwingine jioni, 5 [g]kila mmoja atolewe
pamoja na sadaka ya nafaka sehemu ya
kumi ya efa[h] ya unga laini uliochanganywa
pamoja na robo ya hini[i] ya mafuta ya
zeituni. 6 [j]Hii ni sadaka ya kawaida ya
kuteketezwa iliyoanzishwa katika Mlima
Sinai kama harufu nzuri ya kupendeza,
sadaka iliyotolewa kwa BWANA kwa moto.
7 [k]Sadaka ya kinywaji itakayotolewa pamoja
na kila mwana-kondoo ni robo ya hini ya
kinywaji kilichochachuka. Mimina sadaka
ya kinywaji kwa BWANA mahali patakatifu.
8 [l]Andaa yule mwana-kondoo wa pili jioni,
pamoja na sadaka ya nafaka na sadaka
ya kinywaji kama ulivyofanya kwa ile
sadaka nyingine ya asubuhi. Hii ni sadaka
iliyotolewa kwa kuteketezwa kwa moto,
harufu nzuri ya kumpendeza BWANA.

*Sadaka Za Sabato*

9 [m]" 'Siku ya Sabato, utatoa sadaka ya
wana-kondoo wawili wa mwaka mmoja
wasiokuwa na dosari pamoja na sadaka yake
ya kinywaji na sadaka ya nafaka yenye uzito
wa sehemu mbili za kumi za efa[n] za unga
laini uliochanganywa na mafuta. 10 [o]Hii ni
sadaka ya kuteketezwa itakayotolewa kwa
ajili ya kila Sabato, pamoja na sadaka ya
kawaida ya kuteketezwa na sadaka yake
ya kinywaji.

*Sadaka Za Kila Mwezi*

11 [p]" 'Siku ya kwanza ya kila mwezi,
mtamletea BWANA sadaka ya kuteketezwa
ya fahali wawili wachanga, kondoo dume
mmoja na wana-kondoo saba wa mwaka
mmoja, wote wasiokuwa na dosari.
12 [q]Pamoja na kila fahali, kutakuwa na
sadaka ya nafaka ya unga laini sehemu tatu
za kumi za efa,[r] uliochanganywa na mafuta,
pamoja na kondoo dume mmoja, sadaka ya
nafaka ya unga laini uliochanganywa na

[a]**27:21** Mwa 25:22; Ay 9:14; Za 106:13; Isa 8:19; 1:13; Mal 2:7; 3:1; Kut 28:30; Yos 9:14; Amu 1:1; 20:18; Law 8:8; Kum 33:8; 1Sam 28:6
[b]21 Urimu na Thumimu maana yake ni Nuru na Kweli; vifaa hivi viliwekwa kwenye kifuko cha juu cha kisibau cha kuhani mkuu ili kujua mapenzi ya Mungu kwenye mambo ya kutatanisha.
[c]**27:23** Kum 3:28; Isa 55:4
[d]**28:2** Law 23:1-44; 3:11; 1:9; Mal 1:7-12
[e]**28:3** Kut 12:3; 29:38; Amo 4:4; Kut 29:38
[f]**28:4** Kut 29:39; 12:6
[g]**28:5** Hes 29:6; Law 6:20; 2:1; Kut 16:36; 29:38-42; Hes 15:4
[h]5 Sehemu ya kumi ya efa ni sawa na kilo moja.
[i]5 Robo ya hini ni sawa na lita moja.
[j]**28:6** Law 1:3; Kut 19:3; Law 1:9
[k]**28:7** Hes 6:15; Law 10:9; 3:7; Hes 3:28; Kut 29:42; 30:9; Law 23:13; Hes 15:5-10; Isa 57:1
[l]**28:8** Kut 29:39; Law 23:7; 1:9
[m]**28:9** Kut 20:10; Mt 12:5; Law 23:13; Eze 46:4; 40:4
[n]9 Sehemu mbili za kumi za efa ni sawa na kilo 2.
[o]**28:10** Law 23:38; 1Sam 20:5; 1Nya 23:31; Neh 10:33; Isa 1:13-14; Eze 45:17; Hos 2:11; Kol 2:16
[p]**28:11** Hes 10:10; 7:15; Law 5:15; 1:3
[q]**28:12** Hes 15:6; 29:3; 15:9
[r]12 Sehemu tatu za kumi za efa ni sawa na kilo 3.

mafuta; 13 [a]pamoja na kila mwana-kondoo,
sadaka ya nafaka yenye uzito wa sehemu ya
kumi ya efa ya unga laini uliochanganywa
na mafuta. Hii ni kwa ajili ya sadaka ya
kuteketezwa, harufu nzuri, sadaka ya
kuteketezwa iliyotolewa kwa moto kwa
BWANA. 14 [b]Pamoja na kila fahali kutakuwa
na sadaka ya kinywaji nusu ya hini[c] ya divai;
pamoja na kila kondoo dume, theluthi moja
ya hini,[d] na pamoja na kila mwana-kondoo
robo hini. Hii ni sadaka ya kuteketezwa ya
kila mwezi itakayotolewa kila mwandamo
wa mwezi kwa mwaka. 15 [e]Zaidi ya sadaka
ya kawaida ya kuteketezwa pamoja na
sadaka yake ya kinywaji, mbuzi mmoja
dume atatolewa kwa BWANA kama sadaka
ya dhambi.

*Pasaka*

**(Walawi 23:5-14)**

16 [f]“ ‘Katika siku ya kumi na nne ya
mwezi wa kwanza, itafanyika Pasaka ya
BWANA. 17 [g]Katika siku ya kumi na tano
ya mwezi huo itakuwa sikukuu; kwa siku
saba mtakula mikate isiyotiwa chachu.
18 [h]Katika siku ya kwanza mtakuwa na
kusanyiko takatifu, msifanye kazi za
kawaida. 19 [i]Leteni mbele za BWANA sadaka
ya kuteketezwa, sadaka ya kuteketezwa
ya mafahali wawili wachanga, kondoo
dume mmoja na wana-kondoo dume saba
wenye umri wa mwaka mmoja, wote wasio
na dosari. 20 [j]Pamoja na kila fahali, andaa
sadaka ya nafaka sehemu tatu za kumi
za efa za unga laini uliochanganywa na
mafuta; pamoja na kondoo dume, andaa
sehemu mbili za kumi za efa; 21 pia pamoja
na kila mmoja wa wale wana-kondoo saba,
andaa sehemu ya kumi ya efa. 22 [k]Pia mtoe
beberu mmoja kama sadaka ya dhambi
ambaye atafanya upatanisho kwa ajili
yenu. 23 Andaa hizi licha ya zile sadaka za
kawaida za kuteketezwa za kila asubuhi.
24 [l]Kwa njia hii andaa chakula cha sadaka ya
kuteketezwa kila siku, kwa siku saba kama
harufu nzuri impendezayo BWANA. Hii
itaandaliwa licha ya ile sadaka ya kawaida
ya kuteketezwa ya kila siku pamoja na
sadaka yake ya kinywaji. 25 [m]Siku ya saba
mwe na kusanyiko takatifu na msifanye kazi
zenu za kawaida.

*Sikukuu Ya Majuma*

**(Walawi 23:15-22)**

26 [n]“ ‘Siku ya malimbuko, mnapomletea
BWANA sadaka ya nafaka mpya wakati wa
Sikukuu ya Majuma, mwe na kusanyiko
takatifu na msifanye kazi zenu za kawaida.
27 [o]Mlete sadaka ya kuteketezwa ya mafahali
wawili wachanga, kondoo dume mmoja,
na pia wana-kondoo saba wenye umri
wa mwaka mmoja, kama harufu nzuri
ya kumpendeza BWANA. 28 Pamoja na
kila fahali itatolewa sadaka ya nafaka ya
unga laini sehemu tatu za kumi za efa
uliochanganywa na mafuta; pamoja na
kondoo dume, andaa sehemu mbili za
kumi za efa za unga laini; 29 na sehemu ya
kumi ya efa ya unga laini kwa kila mmoja
wa wana-kondoo saba. 30 Ongeza beberu
mmoja kwa kufanya upatanisho kwa ajili
yenu. 31 Andaa hizi sadaka pamoja na
sadaka zake za vinywaji, kuwa nyongeza ya
sadaka za kawaida za kuteketezwa, pamoja
na sadaka yake ya nafaka. Hakikisha kuwa
wanyama hao hawana dosari.

---

[a]**28:13** Law 6:14; Hes 15:3; Law 1:9
[b]**28:14** Hes 15:11; 2Nya 2:4; Eze 3:5
[c]14 Nusu ya hini ni sawa na lita 2.
[d]14 Theluthi moja ya hini ni sawa na lita 1.2.
[e]**28:15** Hes 4:3; 29:16
[f]**28:16** Kut 12:11; 2Nya 30:13; 35:1; Kut 12:6; Law 23:5; Lk 22:7
[g]**28:17** Kut 12:19; 12:15
[h]**28:18** Kut 12:16; Law 23:7
[i]**28:19** Law 1:9; 22:20; Hes 29:8; Kum 15:21
[j]**28:20** Law 14:10
[k]**28:22** Law 4:2; 8:3; Hes 15:28; Law 16:18; Rum 8:3; Gal 4:4; Ebr 9:12; 10:1
[l]**28:24** Law 1:9; 2Kor 2:15; Efe 5:2
[m]**28:25** Kut 12:16; 13:6; Law 23:8
[n]**28:26** Kut 34:2; 23:16; Law 23:10; Kum 16:10; Mit 3:9; Mdo 2:1
[o]**28:27** Law 23:18-19

*Sikukuu Ya Tarumbeta*

**(Walawi 23:23-25)**

29 [a]“ ‘Katika siku ya kwanza ya mwezi
wa saba mtakuwa na kusanyiko
takatifu na msifanye kazi ya kawaida. Ni
siku kwa ajili yenu ya kupiga tarumbeta.
2 [b]Mtatayarisha sadaka ya kuteketezwa
kama harufu nzuri impendezayo Bwana
ya fahali mmoja mchanga, kondoo dume
mmoja, na wana-kondoo saba wa mwaka
mmoja, wote wasio na dosari. 3 [c]Pamoja
na fahali, andaeni sadaka ya nafaka
sehemu ya kumi tatu za efa za unga laini
uliochanganywa na mafuta; kwa kondoo
dume, andaa unga sehemu ya kumi mbili za
efa; 4 [d]na pamoja na wana-kondoo saba kila
mmoja aandaliwe na sehemu ya kumi ya
efa ya unga. 5 [e]Ongeza beberu mmoja kama
sadaka ya dhambi kufanya upatanisho kwa
ajili yenu. 6 [f]Hivi ni nyongeza ya sadaka za
kuteketezwa kila mwezi na kila siku pamoja
na sadaka zake za nafaka na sadaka za
vinywaji kama ilivyoainishwa. Ni sadaka
zinazotolewa kwa Bwana kwa moto,
harufu inayopendeza.

*Siku Ya Upatanisho*

**(Walawi 23:26-32)**

7 [g]“ ‘Kwenye siku ya kumi ya mwezi huu
wa saba mtakuwa na kusanyiko takatifu.
Mtajikana wenyewe na msifanye kazi.
8 [h]Toeni sadaka ya kuteketezwa ya fahali
mmoja mchanga, kondoo dume mmoja,
na wana-kondoo saba wa mwaka mmoja,
wote wasio na dosari, kama harufu
nzuri inayompendeza Bwana. 9 [i]Pamoja
na fahali, andaeni sadaka ya nafaka
sehemu ya kumi tatu za efa za unga laini
uliochanganywa na mafuta; pamoja na
kondoo dume, sehemu ya kumi mbili za
efa za unga laini; 10 [j]na kwa kila mmoja wa
wana-kondoo saba andaa sehemu ya kumi
ya unga laini kwa kila mmoja. 11 [k]Ongeza
beberu mmoja kama sadaka ya dhambi,
katika nyongeza ya sadaka ya dhambi kwa
ajili ya upatanisho, na sadaka ya kawaida
ya kuteketezwa pamoja na sadaka yake ya
nafaka, na sadaka zake za vinywaji.

*Sikukuu Ya Vibanda*

**(Walawi 23:33-44)**

12 [l]“ ‘Katika siku ya kumi na tano ya
mwezi wa saba, mtakuwa na kusanyiko
takatifu, na hamtafanya kazi za kawaida.
Adhimisheni sikukuu kwa Bwana kwa
siku saba. 13 [m]Toeni sadaka ya kuteketezwa
mafahali wachanga kumi na watatu, kondoo
dume wawili, na wana-kondoo kumi na
wanne wa mwaka mmoja, wote wasio na
dosari, kama harufu nzuri inayompendeza
Bwana. 14 [n]Pamoja na hao mafahali kumi
na watatu, kila mmoja aandaliwe na sadaka
ya nafaka sehemu ya kumi tatu za efa za
unga laini uliochanganywa na mafuta;
kwa kondoo dume wawili, kila mmoja
aandaliwe sehemu ya kumi mbili za efa za
unga laini; 15 [o]na kwa wana-kondoo kumi
na wanne, kila mmoja aandaliwe sehemu
ya kumi ya efa ya unga laini. 16 [p]Ongeza
beberu mmoja kama sadaka ya dhambi,
kwa nyongeza ya sadaka ya kawaida ya
kuteketezwa, na sadaka yake ya nafaka,
pamoja na sadaka ya vinywaji.
17 [q]“ ‘Katika siku ya pili andaeni mafahali
wachanga kumi na wawili, kondoo dume
wawili, na wana-kondoo kumi na wanne
wa mwaka mmoja, wote wasio na dosari.

[a]**29:1** Hes 28:18
[b]**29:2** Hes 28:2; Law 1:9; Hes 28:11; Law 1:3; Hes 28:3
[c]**29:3** Hes 28:12
[d]**29:4** Hes 28:13
[e]**29:5** Hes 28:15
[f]**29:6** Hes 28:11; 28:3; 28:5; 28:7; Law 1:9; Hes 28:2; Dan 12:11; Law 6:9; Hes 15:11, 12
[g]**29:7** Mdo 27:9; Kut 31:15; Law 16:29; Ezr 8:21; Za 35:13; Isa 58:5; Lk 13:3-4; 1Kor 9:27; Yak 4:9
[h]**29:8** Law 22:20; Hes 28:19; 29:8; Kum 15:21; 17:1
[i]**29:9** Hes 28:12
[j]**29:10** Hes 28:13
[k]**29:11** Hes 28:12; Law 16:3
[l]**29:12** 1Fal 8:2; 12:32; Law 23:24
[m]**29:13** Hes 28:2; 28:3; Ebr 10:1-18; Ezr 3:8; Dan 9:24
[n]**29:14** Hes 15:6
[o]**29:15** Hes 28:13
[p]**29:16** Hes 28:15
[q]**29:17** Law 23:36; Hes 28:3

18 [a]Pamoja na mafahali, kondoo dume,
na wana-kondoo, andaeni sadaka zao za
nafaka na sadaka za vinywaji, kulingana na
idadi iliyoainishwa. 19 [b]Weka beberu mmoja
kama sadaka ya dhambi, kwa nyongeza
ya kawaida ya sadaka ya kuteketezwa, na
sadaka yake ya nafaka, pamoja na sadaka
zao za vinywaji.
20 " 'Katika siku ya tatu andaeni mafahali
wachanga kumi na wawili, kondoo dume
wawili, na wana-kondoo kumi na wanne
wa mwaka mmoja, wote wasio na dosari.
21 Pamoja na mafahali, kondoo dume,
na wana-kondoo, andaeni sadaka zao za
nafaka na sadaka za vinywaji, kulingana na
idadi iliyoainishwa. 22 Weka beberu mmoja
kama sadaka ya dhambi, kwa nyongeza
ya kawaida ya sadaka ya kuteketezwa, na
sadaka yake ya nafaka, pamoja na sadaka
zao za vinywaji.
23 " 'Katika siku ya nne andaeni mafahali
wachanga kumi na wawili, kondoo dume
wawili, na wana-kondoo kumi na wanne
wa mwaka mmoja, wote wasio na dosari.
24 Pamoja na mafahali, kondoo dume,
na wana-kondoo, andaeni sadaka zao za
nafaka na sadaka za vinywaji, kulingana na
idadi iliyoainishwa. 25 Weka beberu mmoja
kama sadaka ya dhambi, kwa nyongeza
ya kawaida ya sadaka ya kuteketezwa, na
sadaka yake ya nafaka, pamoja na sadaka
zao za vinywaji.
26 [c]" 'Katika siku ya tano andaeni mafahali
tisa, kondoo dume wawili na wana-kondoo
kumi na wanne wa mwaka mmoja, wote
wasio na dosari. 27 Pamoja na mafahali,
kondoo dume na wana-kondoo, andaeni
sadaka zao za nafaka na sadaka za kinywaji
kulingana na idadi iliyoainishwa. 28 Ongeza
beberu mmoja kama sadaka ya dhambi
katika nyongeza ya sadaka ya kawaida
ya kuteketezwa na sadaka yake ya nafaka
pamoja na sadaka ya kinywaji.
29 " 'Katika siku ya sita andaeni mafahali
wachanga kumi na wawili, kondoo dume
wawili, na wana-kondoo kumi na wanne
wa mwaka mmoja, wote wasio na dosari.
30 Pamoja na mafahali, kondoo dume,
na wana-kondoo, andaeni sadaka zao za
nafaka na sadaka za vinywaji, kulingana na
idadi iliyoainishwa. 31 Weka beberu mmoja
kama sadaka ya dhambi, kwa nyongeza
ya kawaida ya sadaka ya kuteketezwa, na
sadaka yake ya nafaka, pamoja na sadaka
zao za vinywaji.
32 " 'Katika siku ya saba andaeni mafahali
wachanga kumi na wawili, kondoo dume
wawili, na wana-kondoo kumi na wanne
wa mwaka mmoja, wote wasio na dosari.
33 Pamoja na mafahali, kondoo dume,
na wana-kondoo, andaeni sadaka zao za
nafaka na sadaka za vinywaji, kulingana na
idadi iliyoainishwa. 34 Weka beberu mmoja
kama sadaka ya dhambi, kwa nyongeza
ya kawaida ya sadaka ya kuteketezwa, na
sadaka yake ya nafaka, pamoja na sadaka
zao za vinywaji.
35 [d]" 'Katika siku ya nane mtakuwa na
kusanyiko, na msifanye kazi ya kawaida.
36 Toeni sadaka ya kuteketezwa kama harufu
nzuri inayompendeza BWANA, sadaka ya
kuteketezwa ya fahali mmoja, kondoo
dume mmoja, na wana-kondoo dume saba
wa mwaka mmoja, wote wasio na dosari.
37 Pamoja na fahali, kondoo dume na wana-
kondoo, andaeni sadaka zao za nafaka, na
sadaka za vinywaji, kulingana na idadi
iliyoainishwa. 38 Ongeza beberu mmoja
kama sadaka ya dhambi, katika nyongeza
ya sadaka ya kawaida ya kuteketezwa, na
sadaka yake ya nafaka pamoja na sadaka
ya kinywaji.
39 [e]" 'Zaidi ya kile unachoweka nadhiri
na sadaka zenu za hiari, andaeni hizi kwa
ajili ya BWANA kwenye sikukuu zenu
zilizoamriwa: sadaka zenu za kuteketezwa,
sadaka za nafaka, sadaka za vinywaji,
pamoja na sadaka zenu za amani.' "
40 [f]Mose akawaambia Waisraeli yale yote
BWANA alimwagiza.

[a]**29:18** Hes 28:7, 14; 15:4-12; Law 2:1
[b]**29:19** Hes 28:15; 28:3
[c]**29:26** Yn 1:29; Ebr 7:26; Ufu 5:6-14
[d]**29:35** Law 23:36; Za 47:5-6; Isa 11:10; Ufu 7:9-17; 11:15
[e]**29:39** Hes 36:2; 7:16; 23:2; 1:3; 1Nya 23:31; 2Nya 31:3; Law 3:1
[f]**29:40** Kut 24:3; Kum 5:27-31; Yn 7:19; Mdo 7:37-38; 7:38

*Nadhiri*

30 [a]Mose akawaambia viongozi wa makabila ya Israeli: “Hili ndilo BWANA analoagiza: 2 [b]Mwanaume awekapo nadhiri kwa BWANA, au anapoapa kujifunga kwa ahadi, kamwe asitangue neno lake, bali ni lazima afanye kila kitu alichosema.

3 “Wakati mwanamwali anayeishi bado nyumbani kwa baba yake atakapoweka nadhiri kwa BWANA, ama amejifunga mwenyewe kwa ahadi, 4 na baba yake akasikia kuhusu nadhiri au ahadi yake lakini asimwambie lolote, ndipo nadhiri zake zote na kila ahadi aliyoiweka na kujifunga kwayo itathibitika. 5 Lakini kama baba yake akimkataza wakati anapoisikia, hakuna nadhiri wala ahadi yake yoyote aliyojifunga kwayo itakayosimama; BWANA atamweka huru huyo mwanamwali kwa sababu baba yake amemkataza.

6 [c]“Ikiwa ataolewa baada ya kuweka nadhiri au baada ya midomo yake kutamka ahadi fulani bila kufikiri akawa amejifunga hivyo, 7 na mume wake akasikia habari hiyo asimwambie neno lolote, ndipo nadhiri zake ama ahadi zake ambazo alikuwa amejifunga nazo zitathibitika. 8 [d]Lakini ikiwa mume wake atamkataza atakaposikia kuhusu hilo, atakuwa ametangua nadhiri ambazo zilikuwa zimemfunga mkewe, ama ahadi aliyotamka pasipo kufikiri ambayo amejifunga kwayo, naye BWANA atamweka huru yule mwanamke.

9 [e]“Nadhiri yoyote ama patano ambalo limefanywa na mjane ama mwanamke aliyeachwa vitakuwa vimemfunga.

10 “Ikiwa mwanamke anayeishi na mumewe ataweka nadhiri ama kujifunga mwenyewe kwa ahadi chini ya kiapo, 11 na mumewe akasikia kuhusu jambo hili lakini asimwambie lolote wala hakumkataza, ndipo viapo vyake vyote au ahadi zinazomfunga zitakapothibitika. 12 [f]Lakini ikiwa mumewe atabatilisha nadhiri hizo baada ya kuzisikia, basi hakuna nadhiri au ahadi zozote alizoziweka kwa midomo yake zitakazothibitika. Mumewe atakuwa amezibatilisha, na BWANA atamweka huru yule mwanamke. 13 Mumewe anaweza kuthibitisha au kutangua nadhiri yoyote anayoweka, au ahadi yoyote aliyoweka kwa kuapa ili kujikana mwenyewe. 14 Lakini ikiwa mumewe hasemi lolote kwake kuhusu jambo hilo siku baada ya siku, basi mumewe atakuwa amethibitisha nadhiri zote, na ahadi zote zinazomfunga mkewe. Anavithibitisha kwa kutokusema lolote kwa mkewe anapoyasikia hayo. 15 Hata hivyo, ikiwa mumewe atavibatilisha baada ya kusikia hayo, basi atawajibika kwa hatia ya mkewe.”

16 Haya ndiyo masharti ambayo BWANA alimpa Mose kuhusu mahusiano kati ya mtu na mkewe, na kati ya baba na binti yake ambaye bado anaishi nyumbani kwa baba yake.

*Kulipiza Kisasi Juu Ya Wamidiani*

31 BWANA akamwambia Mose, 2 [g]“Uwalipize kisasi Wamidiani kwa ajili ya Waisraeli. Halafu baada ya hayo, utakufa.”

3 [h]Kwa hiyo Mose akawaambia watu, “Waandaeni baadhi ya wanaume wenu waende vitani kupigana na Wamidiani ili wawalipize kisasi cha BWANA. 4 Peleka wanaume 1,000 vitani kutoka kila kabila la Israeli.” 5 Kwa hiyo waliandaliwa wanaume 12,000 kwa vita, wanaume 1,000 kutoka kila kabila, walitolewa kutoka koo za Israeli. 6 [i]Mose aliwatuma vitani, watu 1,000 kutoka kila kabila, pamoja na Finehasi mwana wa kuhani Eleazari,

---

[a]**30:1** Hes 1:4, 16; 7:2; Kum 1:13, 17
[b]**30:2** Kum 23:21-23; Amu 11:23, 30; Ay 22:27; Za 22:25; 50:14; 61:5; 76:11; 116:14; Mit 20:25; Mhu 5:4; Isa 19:21; Yon 1:16; 2:9; Mwa 28; 20; Law 27:2; Za 56:12; 119:106; Law 5:4
[c]**30:6** Law 5:4
[d]**30:8** Mwa 3:6; 1Kor 7:4; 14:34; Efe 5:22-24; Kol 3:18; 1Tim 2:11-12; 1Pet 3:1
[e]**30:9** Law 21:7
[f]**30:12** Efe 5:22; Kol 3:18
[g]**31:2** Mwa 25:2; Hes 20:26; 25:17; Kum 32:35, 43; Mwa 15:15
[h]**31:3** Amu 11:36; 1Sam 24:12; 2Sam 4:8; 22:48; Za 94:1; 149:7; Isa 34:8; Yer 11:20; 46:10; Eze 25:17; Kum 32:35; Yer 50:28; Za 94:1; Rum 12:19; Ebr 10:30
[i]**31:6** Kut 6:25; Hes 14:44; 10:2; 10:9

ambaye alichukua vyombo vya mahali
patakatifu na tarumbeta za kuashiria.
7 [a]Walipigana dhidi ya Wamidiani, kama
BWANA alivyomwagiza Mose, nao waliua
kila mwanaume. 8 [b]Miongoni mwa watu
waliouawa walikuwepo wafalme watano
wa Midiani, nao ni Evi, Rekemu, Suri,
Huri na Reba. Vilevile walimuua Balaamu
mwana wa Beori kwa upanga. 9 [c]Waisraeli
waliwateka wanawake wa Kimidiani pamoja
na watoto wao na walichukua makundi ya
ng'ombe, kondoo na mali zao kama nyara.
10 [d]Walichoma moto miji yote ambayo
Wamidiani walikuwa wanaishi, pamoja na
kambi zao zote. 11 [e]Walichukua nyara zote
na mateka, pamoja na watu na wanyama,
12 [f]nao waliwaleta wafungwa mateka na
nyara kwa Mose na kwa kuhani Eleazari,
nao Waisraeli walikusanyika kwenye kambi
zao katika tambarare za nchi ya Moabu,
kando ya Yordani ng'ambo ya Yeriko.
13 Mose, kuhani Eleazari na viongozi
wote wa jumuiya wakatoka kuwalaki nje
ya kambi. 14 [g]Mose aliwakasirikia maafisa
wa jeshi, yaani hao wakuu wa jeshi wa
maelfu na wakuu wa jeshi wa mamia,
ambao walirudi kutoka vitani.
15 [h]Mose akawauliza, "Je, mmewaacha
wanawake wote hai?" 16 [i]"Wanawake hao
ndio waliofuata ushauri wa Balaamu, nao
ndio waliowasababisha Waisraeli wamwasi
BWANA kwa kile kilichotokea kule Peori, na
kwa hiyo pigo liliwapata watu wa BWANA.
17 [j]Sasa waue wavulana wote. Pia muue
kila mwanamke ambaye alikwisha fanya
tendo la ndoa, 18 lakini mwacheni hai kwa
ajili yenu kila msichana ambaye kamwe
hajawahi kuzini na mwanaume.
19 [k]"Ninyi nyote ambao mmeua mtu
yeyote au kumgusa mtu yeyote ambaye
ameuawa, lazima mkae nje ya kambi kwa
muda wa siku saba. Katika siku ya tatu na
ya saba lazima mjitakase wenyewe pamoja
na wafungwa wenu. 20 [l]Takaseni kila vazi
pamoja na kila kitu kilichotengenezwa kwa
ngozi, kwa singa za mbuzi au kwa mti."
21 Kisha kuhani Eleazari aliwaambia
askari waliokuwa wamekwenda vitani,
"Haya ndiyo matakwa ya sheria ambayo
BWANA alimpa Mose: 22 [m]Dhahabu, fedha,
shaba, chuma, bati, risasi, 23 [n]na kitu
kingine chochote ambacho kinaweza
kuhimili moto lazima mkipitishe kwenye
moto, kisha kitakuwa safi. Lakini ni lazima
pia kitakaswe kwa maji ya utakaso. Kitu
chochote kisichoweza kuhimili moto lazima
kipitishwe kwenye yale maji ya utakaso.
24 [o]Katika siku ya saba fueni nguo zenu,
nanyi mtakuwa safi. Kisha mtaweza kuingia
kambini."

*Kugawanya Mateka*

25 BWANA akamwambia Mose, 26 [p]"Wewe
na kuhani Eleazari pamoja na viongozi wa
jamaa ya jumuiya mtahesabu watu wote na
wanyama ambao walitekwa. 27 [q]Gawanyeni
hizo nyara kati ya askari ambao walishiriki
katika vita na kwa jumuiya. 28 [r]Kutoka
fungu la wale waliokwenda kupigana vitani,
tenga kama ushuru kwa ajili ya BWANA
kitu kimoja kati ya kila mia tano, ikiwa ni
wanadamu, ng'ombe, punda, kondoo au
mbuzi. 29 Chukua ushuru huu kutoka fungu

---

[a]**31:7** Hes 25:16; Kum 20:13; Amu 21:11; 1Fal 11:15; 1Sam 27:9; 1Fal 11:15-16; Kum 20:13; Amu 21:11; 6:2, 33; 6:1
[b]**31:8** Yos 13:21; Hes 25:15; 22:5; 24:14; Yos 13:22; Za 9:12; Yud 11; Ufu 2:14; 19:20
[c]**31:9** Mwa 34:29
[d]**31:10** Yos 6:24; 8:28; 11:11; Amu 18:27; Mwa 25:16; 1Nya 6:54; Za 69:25; Eze 25:4
[e]**31:11** Kum 20:14; 2Nya 28:8
[f]**31:12** Mwa 49:27; Kut 15:9; Hes 27:2
[g]**31:14** Kut 18:21; Kum 1:15; 2Sam 18:1
[h]**31:15** Kum 2:34; 20:13; Yos 6:21; 8:25; 1Sam 15:3; Yos 10:40; 11:14
[i]**31:16** Hes 22:5; 24:14; 2Pet 2:15; Hes 23:25; 25:1-9; 14:37; Yos 22:17; Za 106:28-29; Hos 9:10; Mik 6:5; Ufu 2:14
[j]**31:17** Kum 7:2; 20:16; Amu 21:11
[k]**31:19** Hes 5:2; 9:6, 10; 19:11, 12, 16; Law 21:1
[l]**31:20** Hes 19:19; Law 11:32
[m]**31:22** Yos 6:19; 22:8
[n]**31:23** 1Kor 3:13; Hes 8:7; 19:9, 17
[o]**31:24** Law 11:25; 14:8; Hes 19:10, 22; Za 51:2; Efe 5:26; Ebr 9:9-10
[p]**31:26** Hes 1:4; 1:19
[q]**31:27** Yos 22:8; 1Sam 25:13; 30:24; Za 68:12
[r]**31:28** Hes 18:21; 2Sam 8:11; 1Nya 8:11; 26:27; Isa 18:7; 23:18; Mt 22:21

lao, umpe kuhani Eleazari kama sehemu ya Bwana. 30 [a]Kutoka fungu la Waisraeli, chukua kitu kimoja kati ya kila hamsini, ikiwa ni wanadamu, ng'ombe, punda, kondoo, mbuzi au wanyama wengine. Hivyo uwape Walawi, ambao wanawajibika kutunza Maskani ya Bwana." 31 Kwa hiyo Mose na kuhani Eleazari wakafanya kama Bwana alivyomwagiza Mose.

32 Nyara zilizobaki kutoka mateka ambayo askari walichukua ni kondoo 675,000, 33 ng'ombe 72,000, 34 punda 61,000, 35 na wanawake 32,000 ambao hawakumjua mume kwa kufanya tendo la ndoa.

36 Nusu ya fungu la wale waliokwenda kupigana vitani lilikuwa:

Kondoo 337,500 37 [b]ambayo ushuru kwa ajili ya Bwana ilikuwa kondoo 675;
38 ng'ombe 36,000 ambao ushuru kwa ajili ya Bwana ulikuwa ng'ombe 72;
39 punda 30,500 ambao ushuru kwa ajili ya Bwana ulikuwa punda 61;
40 Watu 16,000 ambao ushuru kwa ajili ya Bwana ulikuwa watu 32.

41 [c]Mose alimpa kuhani Eleazari ushuru kama sehemu ya Bwana, kama Bwana alivyomwagiza Mose.

42 Ile nusu iliyokuwa ya Waisraeli, ambayo Mose aliitenga kutoka kwa ile ya watu waliokwenda vitani, 43 nusu iliyokuwa ya jumuiya, ilikuwa kondoo 337,500, 44 ng'ombe 36,000, 45 punda 30,500, 46 na wanadamu 16,000. 47 Kutoka hiyo nusu iliyokuwa ya Waisraeli, Mose alichagua moja kati ya kila hamsini ya wanadamu na wanyama, kama Bwana alivyomwagiza, naye aliwapa Walawi, ambao waliwajibika kutunza Maskani ya Bwana.

48 Kisha maafisa waliokuwa juu ya vikosi vya jeshi, wakuu wa jeshi wa maelfu na wakuu wa jeshi wa mamia, walimwendea Mose 49 [d]na kumwambia, "Watumishi wako wamehesabu askari walio chini ya amri yetu na hakuna hata mmoja aliyekosekana. 50 [e]Kwa hiyo tumeleta kama sadaka kwa Bwana vyombo vya dhahabu kila mmoja wetu alivyopata, yaani vikuku, bangili, pete za muhuri, vipuli na mikufu, ili kufanya upatanisho kwa ajili yetu mbele za Bwana."

51 Mose na kuhani Eleazari wakapokea kutoka kwao dhahabu, yaani vyombo vyote vilivyonakshiwa. 52 Dhahabu yote kutoka kwa wakuu wa jeshi wa maelfu na wakuu wa jeshi wa mamia ambavyo Mose na kuhani Eleazari walimletea Bwana kama zawadi ilikuwa shekeli 16,750[f] 53 [g]Kila askari alikuwa amejichukulia nyara zake binafsi. 54 [h]Mose na kuhani Eleazari walipokea dhahabu kutoka kwa wakuu wa jeshi wa maelfu na wakuu wa jeshi wa mamia, wakazileta katika Hema la Kukutania kama ukumbusho kwa Waisraeli mbele za Bwana.

### *Makabila Ng'ambo Ya Yordani*

**(Kumbukumbu 3:12-22)**

32 [i]Kabila la Wareubeni na Wagadi, waliokuwa na makundi makubwa ya ng'ombe, kondoo na mbuzi, waliona kuwa nchi ya Yazeri na nchi ya Gileadi ni nzuri kwa mifugo. 2 [j]Hivyo walimjia Mose, na kuhani Eleazari na viongozi wa jumuiya, na kuwaambia, 3 [k]"Atarothi, Diboni, Yazeri, Nimra, Heshboni, Eleale, Sebamu, Nebo na Beoni, 4 [l]nchi ambayo Bwana ameishinda mbele ya wana wa Israeli, inafaa kwa

[a]**31:30** Hes 3:7; 16:3
[b]**31:37** Law 25:23; Kum 10:14; Za 50:12; Mk 12:17; Lk 20:25; 1Kor 10:26
[c]**31:41** Hes 5:9; 18:8, 19
[d]**31:49** Hes 1:19; Yer 23:4; Kut 23:7; Law 26:7-9; Za 72:14; 116:15; 1Sam 30:19
[e]**31:50** Kut 30:16; Law 17:11; Mt 20:28; Rum 3:25
[f]52 Shekeli 16,750 ni sawa na kilo 200.
[g]**31:53** Mwa 34:29; Kum 20:14
[h]**31:54** Kut 27:21; 40:2; 28:12; Hes 16:40; Kut 30:16; Yos 4:7; Zek 6:14; Lk 22:19; Mdo 1:4
[i]**32:1** Amu 5:16; Hes 21:32; Mwa 31:21; Kut 12:38
[j]**32:2** Law 4:22; Hes 27:2; 2Sam 24:5; Isa 16:8-9
[k]**32:3** Yos 16:2; 18:13; Hes 21:30; Yos 13:27; Hes 21:25; Isa 15:4; 16:9; Yer 48:34; Yos 13:19; Isa 16:8; Yer 48:32; Hes 33:47
[l]**32:4** Hes 21:34; Kut 12:38

mifugo, nao watumishi wako wana
mifugo. 5 [a]Kama tumepata kibali mbele ya
macho yako, nchi hii na ipewe watumishi
wako kama milki yetu. Usitufanye tuvuke
Yordani.”
6 Mose akawaambia Wagadi na
Wareubeni, “Je, watu wa nchi yenu
watakwenda vitani wakati ninyi mmeketi
hapa? 7 [b]Kwa nini mmewakatisha Waisraeli
tamaa wasivuke katika nchi ambayo
Bwana amewapa? 8 [c]Hivi ndivyo baba
zenu walivyofanya wakati nilipowatuma
kutoka Kadesh-Barnea kuipeleleza nchi.
9 [d]Baada ya kufika kwenye Bonde la Eshkoli
na kuitazama nchi, waliwakatisha tamaa
Waisraeli wasiingie katika nchi ambayo
Bwana alikuwa amewapa. 10 [e]Siku ile hasira
ya Bwana iliwaka naye akaapa kiapo hiki:
11 [f]‘Kwa kuwa hawakunifuata kwa moyo
wote, hakuna mtu yeyote mwenye miaka
ishirini au zaidi ambaye alikuja kutoka
Misri atakayeona nchi niliyoahidi kwa
kiapo kwa Abrahamu, Isaki na Yakobo;
12 [g]hakuna hata mmoja isipokuwa Kalebu
mwana wa Yefune, Mkenizi, na Yoshua
mwana wa Nuni, kwa sababu walimfuata
Bwana kwa moyo wote.’ 13 [h]Hasira ya
Bwana iliwaka dhidi ya Waisraeli na
akawafanya watangetange katika jangwa
kwa miaka arobaini, mpaka kizazi chote
cha wale waliofanya maovu mbele yake
kimeangamia.
14 [i]“Nanyi mko hapa, uzao wa wenye
dhambi, mkisimamia mahali pa baba
zenu na mkimfanya Bwana kuwakasirikia
Waisraeli hata zaidi. 15 [j]Kama mkigeuka na
mkiacha kumfuata, atawaacha tena watu
hawa wote jangwani, na mtakuwa sababu
ya maangamizi yao.”
16 [k]Ndipo wakamjia Mose na kumwambia,
“Tungalitaka kujenga mazizi hapa kwa
ajili ya mifugo yetu na miji kwa ajili ya
wanawake wetu na watoto. 17 [l]Lakini
sisi tuko tayari kuchukua silaha zetu na
kutangulia mbele ya Waisraeli mpaka
tutakapowaleta mahali pao. Wakati huo
wanawake wetu na watoto wataishi katika
miji yenye ngome, kwa ajili ya ulinzi
dhidi ya wenyeji wa nchi. 18 [m]Hatutarudi
nyumbani mwetu mpaka kila Mwisraeli
apokee urithi wake. 19 [n]Hatutapokea urithi
wowote pamoja nao ng’ambo ya Yordani,
kwa sababu urithi wetu umekuja kwetu
upande wa mashariki ya Yordani.”
20 [o]Kisha Mose akawaambia, “Kama
mtafanya jambo hili, kama mtajivika silaha
mbele za Bwana kwa ajili ya vita, 21 na
kama ninyi nyote mtakwenda mmejivika
silaha ng’ambo ya Yordani mbele za Bwana
mpaka awe amewafukuza adui zake mbele
zake, 22 [p]hadi wakati nchi itakapokuwa
imeshindwa mbele za Bwana, ndipo
mtaweza kurudi na kuwa huru kutoka
masharti yenu kwa Bwana na Israeli.
Nayo nchi hii itakuwa milki yenu mbele
za Bwana.
23 [q]“Lakini mkishindwa kufanya hili,
mtakuwa mnatenda dhambi dhidi ya
Bwana; nanyi kuweni na hakika kuwa
dhambi yenu itawapata. 24 [r]Jengeni miji
kwa ajili ya wanawake na watoto wenu, na
mazizi kwa ajili ya mbuzi na kondoo zenu,
lakini fanyeni yale mliyoahidi.”
25 [s]Wagadi na Wareubeni wakamwambia
Mose, “Sisi watumishi wako tutafanya kama

[a]**32:5** Hes 13:29
[b]**32:7** Hes 13:27–14:4
[c]**32:8** Hes 13:3; Kum 1:19-25; 1:22
[d]**32:9** Hes 13:23; Kum 1:24
[e]**32:10** Hes 11:1; 14:20-23; 14:11; Za 95:11; Eze 20:15; Ebr 3:8-19
[f]**32:11** Kut 30:14; Hes 1:1; 14:23; Kum 1:35; Hes 14:24; 14:28
[g]**32:12** Hes 14:24; Za 63:8; Kum 1:35; Yos 14:8, 9; Ay 4:7; Za 37:29; Mit 11:31
[h]**32:13** Kut 4:14; Hes 14:28-35; 26:64, 65
[i]**32:14** Kum 1:34; Za 78:59
[j]**32:15** Kum 30:17-18; 2Nya 7:20; Yos 22:16, 18; 2Nya 15:2
[k]**32:16** 1Sam 24:3; Za 50:9; 78:70; Kut 12:38; Kum 3:19
[l]**32:17** Kum 3:18; Yos 4:12, 13; Hes 22:4; Kum 3:20
[m]**32:18** Yos 22:1-4
[n]**32:19** Hes 21:33; Yos 12:1; 22:7
[o]**32:20** Kum 3:18; Yos 4:12-13
[p]**32:22** Yos 22:4; Law 14:34; Kum 3:18-20
[q]**32:23** Mwa 4:7; Isa 3:9; Mwa 44:16; Za 140:11; Mit 13:21; Isa 59:12; Rum 2:9
[r]**32:24** Hes 30:2; 32:16, 34
[s]**32:25** Yos 1:16; 22:2

bwana wetu anavyotuagiza. 26 [a]Watoto na
wake zetu, makundi ya mbuzi na kondoo,
na makundi ya ng'ombe zetu, watabaki
hapa katika miji ya Gileadi. 27 [b]Lakini
watumishi wenu, kila mwanaume aliyevaa
silaha za vita, watavuka ng'ambo kupigana
mbele za BWANA, sawa kama bwana wetu
anavyosema."

28 [c]Kisha Mose akatoa amri kuhusu wao
kwa kuhani Eleazari, na Yoshua mwana wa
Nuni na viongozi wa jamaa za makabila
ya Waisraeli. 29 [d]Mose akawaambia, "Ikiwa
Wagadi na Wareubeni, kila mwanaume
aliyevaa silaha za vita, atavuka Yordani
pamoja nanyi mbele za BWANA, basi wakati
mtakapoishinda nchi iliyoko mbele yenu,
wapeni nchi ya Gileadi kama milki yao.
30 Lakini kama hawatavuka pamoja nanyi
wakiwa wamevaa silaha za vita, lazima
wakubali kupokea milki yao pamoja nanyi
katika nchi ya Kanaani."

31 Wagadi na Wareubeni wakajibu,
"Watumishi wako watafanya lile BWANA
alilosema. 32 [e]Tutavuka mbele za BWANA
kuingia Kanaani tukiwa tumevaa silaha
za vita, lakini mali tutakayoirithi itakuwa
ng'ambo hii ya Yordani."

33 [f]Kisha Mose akawapa Wagadi,
Wareubeni, na nusu ya kabila la Manase
mwana wa Yosefu ufalme wa Sihoni mfalme
wa Waamori, na ufalme wa Ogu mfalme wa
Bashani, nchi yote pamoja na miji yake, na
nchi inayowazunguka.

34 [g]Wagadi wakajenga Diboni, Atarothi,
Aroeri, 35 [h]Atroth-Shofani, Yazeri, Yogbeha,
36 Beth-Nimra na Beth-Harani kama miji
iliyozungushiwa ngome, tena wakajenga
mazizi kwa ajili ya makundi yao ya mbuzi na
kondoo. 37 [i]Nao Wareubeni wakajenga upya
miji ya Heshboni, Eleale na Kiriathaimu,
38 [j]pia Nebo na Baal-Meoni (majina ya
hiyo miji yalibadilishwa) na Sibma. Miji
waliyoijenga upya waliipa majina.

39 [k]Wazao wa Makiri mwana wa Manase
walikwenda Gileadi, wakaiteka nchi na
kuwafukuza Waamori waliokuwa huko.
40 [l]Kwa hiyo Mose akawapa Wamakiri,
wazao wa Manase, nchi ya Gileadi, nao
wakakaa huko. 41 [m]Yairi, mzao wa Manase,
akateka makao yao, akayaita Hawoth-Yairi.
42 [n]Naye Noba akateka Kenathi na makao
yaliyoizunguka, akayaita Noba kwa jina
lake.

### *Vituo Katika Safari Ya Waisraeli*

33 [o]Hivi ndivyo vituo katika safari ya
Waisraeli walipotoka Misri kwa
vikosi chini ya uongozi wa Mose na Aroni.
2 [p]Kwa agizo la BWANA, Mose aliweka
kumbukumbu ya vituo katika safari yao.
Hivi ndivyo vituo katika safari yao:

> 3 [q]Waisraeli walisafiri kutoka
> Ramesesi katika siku ya kumi na tano
> ya mwezi wa kwanza, siku iliyofuata
> Pasaka. Walitembea kwa ujasiri wazi
> mbele ya Wamisri wote, 4 [r]waliokuwa
> wakizika wazaliwa wao wa kwanza
> wote, ambao BWANA alikuwa
> amewaua katikati yao, kwa kuwa
> BWANA alikuwa ameleta hukumu juu
> ya miungu yao.

[a]**32:26** Yos 1:14; 12:2; 22:9; 2Sam 2:9; 1Nya 5:9
[b]**32:27** Yos 4:12
[c]**32:28** Kum 3:18; Yos 1:13; Hes 11:28; 1:16
[d]**32:29** Hes 22:4
[e]**32:32** Yos 12:6
[f]**32:33** Yos 13:24-28; 1Sam 13:7; Yos 1:12; Hes 21:21; Kum 2:26; Yos 12:5; Hes 21:24; 34:24; Kum 2:36; Yos 12:6
[g]**32:34** Kum 2:36; 3:13; 4:48; Yos 12:2; 13:9; Amu 11:26; 1Sam 30:28; 1Nya 5:8; Yer 48:19; Hes 33:45
[h]**32:35** Amu 8:11
[i]**32:37** Hes 21:25; Yos 13; 19; 1Nya 6:76; Yer 48:1; Eze 25:9
[j]**32:38** Isa 15:2; 46:1; Yer 48:1, 22; Hes 32:3; Kut 23:13
[k]**32:39** Mwa 50:23; Hes 26:29; Kum 2:36; Mwa 10:16; Yos 17:1
[l]**32:40** Mwa 50:23; Kum 3:15
[m]**32:41** Kum 3:14; Yos 13:30; Amu 10:4; 1Nya 2:23
[n]**32:42** 1Nya 2:23; Amu 8:11; 1Sam 15:12; 2Sam 18:18
[o]**33:1** Kut 17:1; 40:36; Hes 1:1; Kut 4:16; 6:26
[p]**33:2** Kut 17:4
[q]**33:3** Hes 10:2; Mwa 47:11; Yos 5:10; Kut 14:8; 1:11; 12:37; 12:2; 13:4; Za 105:38; Isa 52:12; Kut 14:8
[r]**33:4** Kut 4:23; 2Nya 24:24; Yer 15:3; Eze 14:21; Kut 12:12; Isa 19:1; Sef 2:11; Ufu 12:8

5 [a]Waisraeli waliondoka Ramesesi na
kupiga kambi huko Sukothi.
6 [b]Wakaondoka Sukothi na kupiga
kambi huko Ethamu, pembeni mwa
jangwa.
7 [c]Wakaondoka Ethamu, wakageuka
wakarudi Pi-Hahirothi, hadi mashariki
ya Baal-Sefoni, wakapiga kambi yao
karibu na Migdoli.
8 [d]Wakaondoka Pi-Hahirothi
wakapita katikati ya bahari mpaka
jangwani, na baada ya kusafiri kwa
siku tatu katika Jangwa la Ethamu,
walipiga kambi huko Mara.
9 [e]Wakaondoka Mara wakaenda
Elimu, mahali ambapo palikuwa na
chemchemi kumi na mbili na mitende
sabini, huko wakapiga kambi.
10 [f]Wakaondoka Elimu na kupiga
kambi kando ya Bahari ya Shamu.
11 [g]Wakaondoka kando ya Bahari ya
Shamu na kupiga kambi katika Jangwa
la Sini.
12 Wakaondoka katika Jangwa la
Sini, wakapiga kambi huko Dofka.
13 Wakaondoka Dofka, wakapiga
kambi huko Alushi.
14 [h]Wakaondoka Alushi, wakapiga
kambi Refidimu, mahali ambapo
hapakuwa na maji kwa ajili ya watu
kunywa.
15 [i]Wakaondoka Refidimu na kupiga
kambi katika Jangwa la Sinai.
16 [j]Wakaondoka katika Jangwa
la Sinai na kupiga kambi huko
Kibroth-Hataava.
17 [k]Wakaondoka Kibroth-Hataava na
kupiga kambi huko Haserothi.
18 [l]Wakaondoka Haserothi na kupiga
kambi huko Rithma.
19 Wakaondoka Rithma na kupiga
kambi huko Rimon-Peresi.
20 [m]Wakaondoka Rimon-Peresi na
kupiga kambi huko Libna.
21 Wakaondoka Libna na kupiga
kambi huko Risa.
22 Wakaondoka Risa na kupiga
kambi huko Kehelatha.
23 Wakaondoka Kehelatha na kupiga
kambi kwenye mlima Sheferi.
24 Wakaondoka kwenye mlima
Sheferi na kupiga kambi huko Harada.
25 Wakaondoka Harada na kupiga
kambi huko Makelothi.
26 Wakaondoka Makelothi na kupiga
kambi huko Tahathi.
27 Wakaondoka Tahathi na kupiga
kambi huko Tera.
28 Wakaondoka Tera na kupiga
kambi huko Mithka.
29 Wakaondoka Mithka na kupiga
kambi huko Hashmona.
30 [n]Wakaondoka Hashmona na
kupiga kambi Moserothi.
31 [o]Wakaondoka Moserothi na kupiga
kambi huko Bene-Yakani.
32 [p]Wakaondoka Bene-Yakani na
kupiga kambi huko Hor-Hagidgadi.
33 [q]Wakaondoka Hor-Hagidgadi na
kupiga kambi huko Yotbatha.
34 Wakaondoka Yotbatha na kupiga
kambi huko Abrona.
35 [r]Wakaondoka Abrona na kupiga
kambi huko Esion-Geberi.
36 [s]Wakaondoka Esion-Geberi na
kupiga kambi huko Kadeshi katika
Jangwa la Sini.

---

[a]**33:5** Kut 12:37
[b]**33:6** Kut 13:20; Mwa 33:17; Yos 13:27; Za 60:6
[c]**33:7** Kut 13:17, 18; 14:2, 9
[d]**33:8** Kut 14:2; 14:22; 15:23
[e]**33:9** Kut 15:27
[f]**33:10** Kut 16:1
[g]**33:11** Kut 16:1; 17:1
[h]**33:14** Kut 15:22; 17:2
[i]**33:15** Kut 17:1; 19:1
[j]**33:16** Hes 11:34
[k]**33:17** Hes 11; 35; Kum 9:22
[l]**33:18** Hes 12:16; Kum 1:1
[m]**33:20** Yos 10:29; 12:15; 15:42; 21:13; 2Fal 8:22; 19:8; 23:31; 1Nya 6:57; 2Nya 21:10; Isa 37:8; Yer 52:1
[n]**33:30** Kum 10:6
[o]**33:31** Kum 10:6
[p]**33:32** Mwa 36:27; Kum 10:6; 1Nya 1:42
[q]**33:33** Kum 10:7
[r]**33:35** Kum 2:8; 1Fal 9:26; 22:48
[s]**33:36** Hes 13:21; 20:1; Kum 32:51; Yos 15:1

37 [a]Wakaondoka Kadeshi na kupiga
kambi kwenye Mlima Hori, mpakani
mwa Edomu. 38 [b]Kwa amri ya BWANA,
kuhani Aroni alipanda Mlima Hori,
mahali alipofia katika siku ya kwanza
ya mwezi wa tano, mwaka wa arobaini
baada ya Waisraeli kutoka Misri.
39 Aroni alikufa juu ya Mlima Hori
akiwa na umri wa miaka 123.

40 [c]Mfalme Mkanaani wa Aradi,
ambaye aliishi huko Negebu ya
Kanaani, akasikia kwamba Waisraeli
wanakuja.

41 Wakaondoka kwenye mlima Hori
na kupiga kambi huko Salmona.

42 Wakaondoka Salmona, wakapiga
kambi huko Punoni.

43 [d]Wakaondoka Punoni, wakapiga
kambi huko Obothi.

44 [e]Wakaondoka Obothi, wakapiga
kambi huko Iye-Abarimu, mipakani
mwa Moabu.

45 [f]Wakaondoka Iye-Abarimu,
wakapiga kambi huko Dibon-Gadi.

46 [g]Wakaondoka Dibon-Gadi na
kupiga kambi huko Almon-Diblathaimu.

47 [h]Wakaondoka Almon-Diblathaimu
na kupiga kambi katika milima ya
Abarimu, karibu na Nebo.

48 [i]Wakaondoka kwenye milima ya
Abarimu na kupiga kambi kwenye
tambarare ya Moabu, kando ya Yordani
ng'ambo ya Yeriko. 49 [j]Huko kwenye
tambarare za Moabu walipiga kambi
kandokando ya Mto Yordani, kuanzia
Beth-Yeshimothi mpaka Abel-Shitimu.

50 [k]Katika tambarare za Moabu kando
ya Yordani kuvukia Yeriko, BWANA
akamwambia Mose, 51 [l]"Sema na Waisraeli
uwaambie: 'Mtakapovuka Mto Yordani
kuingia Kanaani, 52 [m]wafukuzeni wakazi
wote wa nchi iliyo mbele yenu. Haribuni
sanamu zao zote za kuchongwa, na sanamu
zilizotengenezwa kwa kuyeyusha chuma,
na kupabomoa mahali pao pa ibada.
53 [n]Mtaimiliki nchi hiyo na kukaa huko,
kwa kuwa nimewapeni ninyi kuimiliki.
54 [o]Mtaigawanya nchi hiyo kwa kupiga
kura, kufuatana na koo zenu. Kwa kundi
kubwa zaidi toa urithi mkubwa zaidi,
na kwa kundi dogo zaidi urithi mdogo
zaidi. Chochote kinachowaangukia kwa
kura kitakuwa chao. Mtaigawanya nchi
kufuatana na makabila ya babu zenu.

55 [p]" 'Lakini kama hamkuwafukuza
wenyeji wakaao katika nchi hiyo, wale
mtakaowaruhusu wabaki watakuwa kama
sindano kwenye macho yenu na miiba
kwenu kila upande. Watawasumbua katika
nchi mtakayoishi. 56 [q]Kisha nitawatenda
ninyi kile ambacho nimepanga kuwatenda
wao.' "

*Mipaka Ya Kanaani*

34 BWANA akamwambia Mose,
2 [r]"Waamuru Waisraeli na uwaambie:
'Mtakapoingia nchi ya Kanaani, nchi
ambayo itagawanywa kwenu kama urithi
itakuwa na mipaka ifuatayo:

[a]**33:37** Hes 20:22; Mwa 36:16; Hes 20:16
[b]**33:38** Hes 27:13; Kut 16:35; Hes 20:25-28; Kum 10:6; 32:50
[c]**33:40** Mwa 10:18; Hes 21:1; Mwa 12:9; Amu 1:16
[d]**33:43** Hes 21:10
[e]**33:44** Hes 21:11
[f]**33:45** Hes 32:34
[g]**33:46** Yer 48:22; Eze 6:14
[h]**33:47** Hes 27:12; 32:3; Kum 32:49
[i]**33:48** Hes 27:12; 26:3; Mwa 13:10; Hes 22:1; Yos 12:9
[j]**33:49** Yos 12:3; 13:20; Eze 25:9; Hes 21:16
[k]**33:50** Hes 33:48; 34:2
[l]**33:51** Kum 7:1; 9:1; Yos 3:17
[m]**33:52** Law 26:1; Za 106:34-36; Kut 23:24; 34:12-17; Kum 7:2-5, 25, 26; Yos 11:12; 23:7; Amu 2:2
[n]**33:53** Kum 11:31; 17:14; Yos 1:11; 21:43; Za 24:1; Ay 14:11; Dan 4:35
[o]**33:54** Law 16:8; Hes 36:2; 26:54; 35:8; Yos 18:10
[p]**33:55** Yos 23:13; Amu 2:3; Za 106:36; Isa 55:13; Eze 2:6; 28:24; Mik 7:4; 2Kor 12:7; Kut 23:33; Mwa 17:8; Kum 1:7; Za 78:55; 105:11
[q]**33:56** Hes 14:28
[r]**34:2** Hes 33:51; Mwa 17:8; Kum 1:7-8; Yos 23:4; Za 78:54-55; 105:11; Eze 47:15

3 [a]“ ‘Upande wenu wa kusini utajumuisha
sehemu ya Jangwa la Sini kufuata mpaka
wa Edomu. Upande wa mashariki mpaka
wenu wa kusini utaanzia mwisho wa Bahari
ya Chumvi,[b] 4 [c]katiza kusini mwa Pito la
Akrabimu, endelea mpaka Sini na kwenda
kusini ya Kadesh-Barnea. Kisha mpaka huo
utaenda hadi Hasar-Adari hadi Azmoni,
5 [d]mahali ambapo utapinda, na kuunganika
na Kijito cha Misri na kumalizikia kwenye
Bahari ya Kati.[e]
6 [f]“ ‘Mpaka wenu wa magharibi utakuwa
Bahari ya Kati. Huu utakuwa mpaka wenu
upande wa magharibi.
7 [g]“ ‘Kwa mpaka wenu wa kaskazini,
wekeni alama kuanzia Bahari ya Kati hadi
mlima Hori, 8 [h]na kutoka mlima Hori hadi
Pito la Hamathi. Kisha mpaka utaenda hadi
Sedadi, 9 [i]kuendelea hadi Zifroni, na kuishia
Hasar-Enani. Huu utakuwa mpaka wenu
upande wa kaskazini.
10 [j]“ ‘Kwa mpaka wenu wa mashariki,
wekeni alama kuanzia Hasar-Enani hadi
Shefamu. 11 [k]Mpaka utaelekea kusini kuanzia
Shefamu hadi Ribla upande wa mashariki
wa Aini, na kuendelea kwenye miteremko
mashariki mwa Bahari ya Kinerethi.[l] 12 Kisha
mpaka utashuka kuelekea Mto Yordani na
kuishia katika Bahari ya Chumvi.
“ ‘Hii itakuwa nchi yenu, ikiwa na mipaka
yake kila upande.’ ”
13 [m]Mose akawaamuru Waisraeli:
“Gawanyeni nchi hii kwa kura kama urithi.
Bwana ameagiza kwamba itolewe kwa yale
makabila tisa na nusu, 14 [n]kwa sababu jamaa
ya kabila la Reubeni, kabila la Gadi, na nusu
ya kabila la Manase wamekwishapokea
urithi wao. 15 Haya makabila mawili na
nusu wamekwishapokea urithi wao upande
wa mashariki wa Yordani ng’ambo ya
Yeriko, kuelekea mawio ya jua.”
16 Bwana akamwambia Mose, 17 [o]“Haya
ndiyo majina ya watu ambao watakusaidia
kugawanya nchi kama urithi: Eleazari
kuhani na Yoshua mwana wa Nuni. 18 [p]Tena
uteue kiongozi mmoja kutoka kila kabila
kusaidia kuigawanya nchi. 19 [q]Haya ndiyo
majina yao:

“Kalebu mwana wa Yefune,
kutoka kabila la Yuda;
20 [r]Shemueli mwana wa Amihudi,
kutoka kabila la Simeoni;
21 [s]Elidadi mwana wa Kisloni,
kutoka kabila la Benyamini;
22 Buki mwana wa Yogli,
kiongozi kutoka kabila la Dani;
23 [t]Hanieli mwana wa Efodi,
kiongozi kutoka kabila la Manase
mwana wa Yosefu;
24 [u]Kemueli mwana wa Shiftani,
kiongozi kutoka kabila la Efraimu
mwana wa Yosefu;
25 [v]Elisafani mwana wa Parnaki,
kiongozi kutoka kabila la
Zabuloni;
26 Paltieli mwana wa Azani,
kiongozi kutoka kabila la Isakari;
27 [w]Ahihudi mwana wa Shelomi,
kiongozi kutoka kabila la Asheri;
28 Pedaheli mwana wa Amihudi,

---

[a]**34:3** Hes 15:21; Yos 15:1-3; Mwa 14:3; Eze 47:13; Mwa 14:3; Yos 3:16
[b]3 Yaani Bahari Mfu.
[c]**34:4** Yos 15:3; Amu 1:36; Hes 32:8; Yos 15:4
[d]**34:5** Mwa 15:18; 1Fal 8:65; Isa 27:12
[e]5 Yaani Mediterania.
[f]**34:6** Yos 1:4; 9:1; 15:12; 23:4; Eze 47:10; 48:28; 47:9-20
[g]**34:7** Eze 47:15-17; Hes 20:22
[h]**34:8** Hes 13:21; Yos 13:5; 2Sam 8:9; 2Fal 18:25; Isa 10:9; Yer 39:5; Eze 47:15-20
[i]**34:9** Eze 47:17
[j]**34:10** Yos 15:5
[k]**34:11** 2Fal 23:33; 25:6; Yer 39:5; 52:9; Yos 15:32; 21:16; 1Nya 4:32; Kum 3:17; Yos 11:2; 13:27
[l]11 Yaani Bahari ya Galilaya.
[m]**34:13** Law 16:8; Yos 18:10; Mik 2:5; Yos 13:6; 14:1-5; Isa 49:8
[n]**34:14** Hes 32:19; Kum 33:21; Yos 14:3
[o]**34:17** Hes 11:28; Kum 1:38; Kut 6:23-25
[p]**34:18** Hes 1:4; Yos 14:1
[q]**34:19** Hes 26:65; Mwa 29:35; Kum 33:7; Za 60:7; 108:8; Hes 13:6, 30; Kum 1:36
[r]**34:20** Mwa 29:33; 49:5; Eze 48:24
[s]**34:21** Mwa 49:27; Amu 5:14; Za 68:27
[t]**34:23** Hes 1:34; Mwa 48:8-22; Kum 33:13; Mwa 49:22; Za 80:1
[u]**34:24** Hes 1:32
[v]**34:25** Mwa 30:20
[w]**34:27** Hes 1:40

kiongozi kutoka kabila la Naftali."

29 [a]Hawa ndio watu ambao BWANA
aliamuru wagawanye urithi kwa Waisraeli
katika nchi ya Kanaani.

### *Miji Kwa Ajili Ya Walawi*

35 [b]BWANA akamwambia Mose katika
nchi tambarare ya Moabu, kando ya
Mto Yordani kuvukia Yeriko, 2 [c]"Waagize
Waisraeli kuwapa Walawi miji ya kuishi
kutoka urithi ambao Waisraeli wataumiliki.
Wape maeneo ya malisho kuzunguka hiyo
miji. 3 [d]Kisha watakuwa na miji ya kuishi
na maeneo ya malisho kwa ajili ya ng'ombe
zao, mbuzi, kondoo na mifugo yao mingine
yote.
4 "Maeneo ya malisho kuzunguka miji
hiyo ambayo mtawapa Walawi yataenea
mita 450 kutoka kwenye ukuta wa miji.
5 [e]Nje ya mji, pima mita 900 upande wa
mashariki, upande wa kusini mita 900,
upande wa magharibi mita 900, na upande
wa kaskazini mita 900, na mji utakuwa
katikati. Eneo hili litakuwa lao kwa ajili
ya malisho.

### *Miji Ya Makimbilio*

**(Kumbukumbu 19:1-13; Yoshua 20:1-9)**

6 [f]"Miji sita mtakayowapa Walawi itakuwa
ya makimbilio, ambayo mtu anayemuua
mwenzake aweza kukimbilia humo. Zaidi
ya hiyo, wapeni miji mingine arobaini na
miwili. 7 [g]Kwa jumla inawapasa kuwapa
Walawi miji arobaini na minane, pamoja
na maeneo ya malisho yao. 8 [h]Miji ambayo
mtawapa Walawi kutoka nchi ambayo
Waisraeli wanamiliki itatolewa kwa uwiano
wa urithi wa kila kabila. Chukua miji mingi
kutoka lile kabila lenye miji mingi, lakini
uchukue miji michache kutoka kwa kabila
lile lenye miji michache."
9 Kisha BWANA akamwambia Mose:
10 [i]"Sema na Waisraeli, uwaambie:
'Mtakapovuka Yordani kuingia Kanaani,
11 [j]chagueni baadhi ya miji iwe miji yenu
ya makimbilio, ambayo mtu ambaye
ameua mwenzake bila kukusudia aweza
kukimbilia humo. 12 [k]Itakuwa mahali
pa kukimbilia kutoka mlipiza kisasi, ili
kwamba mtu aliyeshtakiwa kwa mauaji
asife kabla ya kujitetea mbele ya mkutano.
13 Miji hii sita mtakayoitoa itakuwa miji
yenu ya makimbilio. 14 [l]Mtatoa miji mitatu
ng'ambo hii ya Yordani na miji mingine
mitatu upande wa Kanaani kama miji ya
makimbilio. 15 [m]Miji hii sita itakuwa mahali
pa makimbilio kwa ajili ya Waisraeli,
wageni na watu wengine wanaoishi katikati
yenu, ili kwamba mtu yeyote ambaye
ameua mtu mwingine pasipo kukusudia
aweze kukimbilia humo.
16 [n]" 'Kama mtu akimpiga mwenzake kwa
chuma naye mtu huyo akafa, mtu huyo
ni muuaji; muuaji sharti atauawa. 17 Au
kama mtu analo jiwe mkononi mwake
ambalo laweza kuua, naye akampiga
mwenzake akafa, yeye ni muuaji; muuaji
huyo sharti atauawa. 18 Au kama mtu
ana chombo cha mti mkononi mwake
ambacho chaweza kuua, naye akampiga
mwenzake akafa, yeye ni muuaji; muuaji
huyo sharti atauawa. 19 Mlipiza kisasi cha
damu atamuua muuaji; wakati akikutana
naye, atamuua. 20 [o]Ikiwa mtu ana chuki ya
siku nyingi na mwenzake akamsukuma au
akamtupia kitu kwa kukusudia naye akafa,
21 [p]au ikiwa katika uadui akampiga ngumi
naye akafa, mtu yule sharti atauawa; yeye

---

[a]**34:29** Kum 32:8; Mdo 17:26
[b]**35:1** Hes 22:1
[c]**35:2** Law 25:32-34; Yos 14:3; 21:1-42; Hes 18:20-24; Kum 18:1-2; 1Nya 6:64; Eze 48:8
[d]**35:3** Kum 18:6; Yos 14:4; 21:2
[e]**35:5** Yos 3:4; Law 25:34; 2Nya 11:14; 13:9; 23:2; 31:19
[f]**35:6** Yos 21:13; Kum 4:41; Za 9:9; 62:7-8; Isa 4:6
[g]**35:7** Yos 21:41
[h]**35:8** Hes 26:54; 33:54; Yos 21:3; Kut 16:18
[i]**35:10** Hes 33:51; Kum 9:1; Yos 1:2; Kum 19:2; Yos 20:2
[j]**35:11** Kut 21:13
[k]**35:12** Kum 19:6; Yos 20:3; 2Sam 14:11
[l]**35:14** Kum 4:41; 2Kor 8:13-14
[m]**35:15** Hes 15:16
[n]**35:16** Kut 21:12; Law 24:17; Kum 19:11-12
[o]**35:20** Kut 21:14; Mwa 4:8; 2Sam 3:37; 1Fal 2:31; Lk 4:29; 1Sam 18:10; Za 10:7-10
[p]**35:21** Kut 21:14

ni muuaji. Mlipiza kisasi cha damu atamuua
muuaji atakapokutana naye.
22 [a]“ ‘Lakini kama mtu akimsukuma
mwenziwe ghafula pasipo chuki, au
kumtupia kitu pasipo kukusudia, 23 au,
pasipo kumwona, akimwangushia jiwe
ambalo laweza kumuua naye akafa, basi kwa
kuwa hakuwa adui yake naye hakukusudia
kumuumiza, 24 [b]kusanyiko lazima liamue
kati yake na mlipiza kisasi wa damu
kufuatana na sheria hizi. 25 [c]Kusanyiko ni
lazima limlinde yule anayeshtakiwa kuua
kutoka kwa mlipiza kisasi wa damu, na
kumrudisha katika mji wa makimbilio
alikokuwa amekimbilia. Lazima akae humo
mpaka atakapokufa kuhani mkuu ambaye
alikuwa amepakwa mafuta matakatifu.
26 “ ‘Lakini kama mshtakiwa atatoka nje
ya mipaka ya mji wa makimbilio ambao
amekimbilia, 27 [d]na mlipiza kisasi wa damu
akamkuta nje ya mji, mlipiza kisasi wa
damu anaweza kumuua mshtakiwa huyo
bila kuwa na hatia ya kuua. 28 Mshtakiwa
lazima akae katika mji wake wa makimbilio
mpaka atakapokufa kuhani mkuu; atarudi
tu kwenye mali yake baada ya kifo cha
kuhani mkuu.
29 [e]“ ‘Hizi ndizo kanuni za sheria
zitakazohitajiwa kwenu na katika vizazi
vyenu vijavyo, popote mtakapoishi.
30 [f]“ ‘Yeyote anayeua mtu atauawa
kama muuaji ikiwa tu kuna ushuhuda wa
mashahidi. Lakini hakuna mtu atakayeuawa
kwa ushuhuda wa shahidi mmoja tu.
31 [g]“ ‘Usikubali fidia yoyote ya kuokoa
uhai wa muuaji ambaye anastahili kufa.
Mtu huyo hakika lazima auawe.
32 [h]“ ‘Usikubali fidia ya mtu yeyote ambaye
amekimbilia katika mji wa makimbilio na
kumruhusu kurudi kuishi katika nchi yake
kabla ya kifo cha kuhani mkuu.
33 [i]“ ‘Msiinajisi nchi mnayoishi. Umwagaji
damu hunajisi nchi, na upatanisho
hauwezekani kufanyika katika nchi ambayo
damu imemwagwa, isipokuwa tu kwa damu
ya yule aliyeimwaga damu. 34 [j]Msiinajisi
nchi mnayoishi, ambayo nami ninakaa, kwa
kuwa Mimi, Bwana, ninakaa katikati ya
Waisraeli.’ ”

*Urithi Wa Binti Za Selofehadi*

36 [k]Viongozi wa jamaa ya ukoo wa
Gileadi mwana wa Makiri, mwana
wa Manase, waliokuwa wametoka
katika koo za wazao wa Yosefu, walikuja
na kuzungumza mbele ya Mose na
viongozi, wakuu wa jamaa ya Waisraeli.
2 [l]Wakasema, “Bwana alipomwamuru
bwana wangu kuwapa Waisraeli nchi
kama urithi kwa kura, alikuamuru kutoa
urithi wa ndugu yetu Selofehadi kwa binti
zake. 3 Sasa ikiwa wataolewa na watu wa
makabila mengine ya Kiisraeli, itakuwa
kwamba urithi wao utaondolewa kutoka
urithi wa mababu zetu na kuongezwa
katika urithi wa kabila ambalo dada hao
wameolewa. Kwa hiyo sehemu ya urithi
tuliyogawiwa itachukuliwa kutoka kwetu.
4 [m]Wakati mwaka wa Yubile kwa Waisraeli
utafika, urithi wao utaongezwa kwa lile
kabila ambalo wameolewa, na mali yao
itaondolewa kutoka urithi wa kabila la
mababu zetu.”
5 [n]Ndipo kwa agizo la Bwana Mose
akatoa amri ifuatayo kwa Waisraeli: “Kile
wazao wa kabila la Yosefu wanachosema ni
kweli. 6 Hivi ndivyo Bwana anavyoamuru
kwa binti za Selofehadi: Wanaweza
kuolewa na mtu yeyote wampendaye,
mradi tu waolewe miongoni mwa koo

---

[a]**35:22** Kut 21:13
[b]**35:24** Yos 20:6
[c]**35:25** Kut 28:41; 29:9; Efe 1:7; Law 4:3; 21:10
[d]**35:27** Kut 22:2
[e]**35:29** Hes 27:11; 10:8; Kut 12:20
[f]**35:30** Kum 17:6; 19:15; Mt 18:16; Yn 7:51; 2Kor 13:1; 1Tim 5:19; Ebr 10:28; Ufu 11:3
[g]**35:31** Kut 21:30; Ay 6:22; Za 49:8; Mit 13:8
[h]**35:32** Mdo 4:12; Gal 2:21
[i]**35:33** Mwa 4:10; Law 18:25; Kum 21:23; Za 106:38
[j]**35:34** Law 18:24-25; Kut 29:45; Kum 21:23; Hes 5:3; Za 76:2; Isa 8:18; Hos 9:3; 2Kor 6:16
[k]**36:1** Hes 26:30; Mwa 50:23; Hes 26:28; 27:2
[l]**36:2** Hes 33:54; 26:33; Yos 17:3-4
[m]**36:4** Law 25:10
[n]**36:5** Hes 27:7

za kabila za baba yao. [7] [a]Hakuna urithi
katika Israeli utakaohamishwa kutoka
kabila moja kwenda kabila jingine, kwa
kuwa kila Mwisraeli atatunza ardhi ya
kabila lake aliyoirithi kutoka kwa baba
zake. [8] [b]Kila binti atakayerithi ardhi katika
kabila lolote la Israeli ni lazima aolewe na
mtu kutoka kabila na ukoo wa baba yake,
ili kila Mwisraeli amiliki urithi wa baba
zake. [9] Hakuna urithi uwezao kuhamishwa
kutoka kabila moja kwenda kabila jingine,
kwa kuwa kila kabila la Israeli litatunza
nchi linayorithi."

[10] Kwa hiyo binti za Selofehadi wakafanya
kama Bwana alivyomwamuru Mose.
[11] [c]Binti za Selofehadi, ambao ni Mahla,
Tirsa, Hogla, Milka na Noa, wakaolewa
na waume, wana wa ndugu za baba yao.
[12] [d]Waliolewa ndani ya koo za wazao wa
Manase mwana wa Yosefu, na urithi wao
ukabaki katika ukoo na kabila la baba yao.

[13] [e]Haya ndiyo maagizo na masharti
ambayo Bwana aliwapa Waisraeli kupitia
Mose katika tambarare za Moabu, karibu
na Yordani ng'ambo ya Yeriko.

---

[a]**36:7** Law 25:23; 1Fal 21:3
[b]**36:8** 1Nya 23:22
[c]**36:11** Hes 27:1
[d]**36:12** 1Nya 7:15
[e]**36:13** Law 7:38; 27:34; Hes 22:1; 26:3; 31:12; Kum 33:4; Neh 9:12-14; Yn 1:17; 7:19

# KUMBUKUMBU LA TORATI

*Amri Ya Kuondoka Mlima Horebu*

1 [a]Haya ni maneno Mose aliyoyasema
kwa Israeli yote jangwani mashariki ya
Yordani, ambayo iko Araba, inayokabiliana
na Sufu, kati ya Parani na Tofeli, Labani,
Haserothi na Dizahabu. 2 [b](Ni mwendo wa
siku kumi na moja kutoka Horebu kwa njia
ya Mlima Seiri mpaka Kadesh-Barnea.)
3 [c]Katika mwaka wa arobaini, siku ya
kwanza ya mwezi wa kumi na moja, Mose
aliwatangazia Waisraeli yale yote BWANA
aliyomwamuru kuwahusu. 4 [d]Hii ilikuwa
baada ya kumshinda Sihoni mfalme wa
Waamori, ambaye alitawala Heshboni, na
pia huko Edrei alikuwa amemshinda Ogu
mfalme wa Bashani, ambaye alitawala
huko Ashtarothi. 5 [e]Huko mashariki ya
Yordani katika nchi ya Moabu, Mose alianza
kuielezea sheria hii, akisema:

6 [f]BWANA Mungu wetu alisema nasi
huko Horebu, "Mmekaa vya kutosha katika
mlima huu. 7 [g]Vunjeni kambi, msonge mbele
kuelekea nchi ya vilima ya Waamori;
nendeni kwa watu wote ambao ni majirani
wa Araba, katika milima, upande wa
magharibi chini ya vilima, katika Negebu
na kandokando ya pwani, mpaka nchi ya
Wakanaani hadi Lebanoni, na kufika mto
mkubwa Frati. 8 [h]Tazama, nimewapa ninyi
nchi hii. Ingieni mkaimiliki nchi ambayo
BWANA aliapa kuwa angaliwapa baba zenu,
Abrahamu, Isaki na Yakobo, pamoja na
vizazi vyao baada yao."

*Uteuzi Wa Viongozi*

**(Kutoka 18:13-27)**

9 [i]Wakati ule niliwaambia, "Ninyi
mmekuwa mzigo mzito sana kwangu
kuwachukua peke yangu. 10 [j]BWANA Mungu
wenu ameongeza hesabu yenu, hivi kwamba
leo ninyi ni wengi kama nyota za angani.
11 [k]Naye BWANA, Mungu wa baba zenu na
awaongeze mara elfu na kuwabariki kama
alivyoahidi! 12 [l]Lakini mimi nitawezaje
kubeba matatizo yenu, na mizigo yenu, na
magomvi yenu peke yangu? 13 [m]Chagueni
baadhi ya watu wenye hekima, wenye
ufahamu na wanaoheshimika kutoka kila
kabila lenu, nami nitawaweka juu yenu."
14 Mlinijibu, "Shauri ulilolitoa ni zuri."
15 [n]Kwa hiyo niliwachukua wanaume
viongozi wa makabila yenu, wenye hekima
na wanaoheshimika, nami nikawateua wawe
na mamlaka juu yenu kama majemadari
wa maelfu, wa mamia, wa hamsini, na wa
makumi, na kama maafisa wa makabila.
16 [o]Nami wakati ule nikawaagiza waamuzi
wenu: Sikilizeni magomvi kati ya ndugu
zenu na mwamue kwa haki, hata kama
shauri ni kati ya ndugu wa Kiisraeli, au
kati ya mmoja wa ndugu wa Kiisraeli na
mgeni. 17 [p]Msionyeshe upendeleo katika
maamuzi; wasikilizeni wote sawasawa,
wadogo kwa wakubwa. Msimwogope mtu
yeyote, kwa kuwa hukumu ni ya Mungu.

[a]**1:1** Hes 13:29; Kum 4:46; 2:8; 3:17; Yos 3:16; 8:14; 11:2; Eze 47:8; Hes 10:12
[b]**1:2** Kut 3:1; Mwa 14:7; Kum 2:14; 9:23; Yos 15:3; Hes 24:18; 1Fal 3:8; 2Kor 11:28
[c]**1:3** Hes 14:33; 32:13; Kum 8:2; Ebr 3:7-9; Mwa 50:3; Kum 34:8; Yos 4:19; Kum 4:1-2
[d]**1:4** Hes 21:21-26; Mwa 10:16; 14:17; Hes 21:25; 21:33-35; Kum 3:10; Yos 9:10; 12:4; 1Nya 11:44
[e]**1:5** Hes 21:11
[f]**1:6** Hes 10:13; Kut 3:1; Kum 2:3
[g]**1:7** Kum 2:24; 7:1; Yos 10:5; Hes 21:1; Yos 11:16; 12:8; 2Sam 24:7; Mwa 10:18; Kum 11:24; Mwa 2:14
[h]**1:8** Yos 23:13; Hes 34:2; Kut 13:11; Hes 14:23; Ebr 6:13-14
[i]**1:9** Hes 11:14; Za 30:4; Kut 18:18
[j]**1:10** Eze 16:7; Kum 7:13; Mwa 15:5; Isa 51:2; 60:22; Eze 33:24; Mwa 22:17; Hes 10:36
[k]**1:11** Kut 32:13; 2Sam 24:3; 1Nya 21:3
[l]**1:12** Kut 5:22; 18:18
[m]**1:13** Mwa 47:6; 1
[n]**1:15** Kut 18:25; 5:14; Hes 11:16; Yos 1:10; 3:2; Mwa 47:6; Hes 31:14; 1Sam 8:12; 22:7; 1Fal 14:27; Hes 1:4
[o]**1:16** 1Fal 3:9; Za 72:1; Mit 2:9; Mwa 31:37; Yn 7:24; Kut 12:19; 22:21
[p]**1:17** Kut 18:16; Law 19:15; Mdo 10:34; Yak 2:1; Mit 29:25; Kut 18:26

Mniletee mimi shauri lolote lililo gumu
sana kwenu, nami nitalisikiliza. 18 [a]Nami
wakati ule niliwaambia kila kitu ambacho
mngefanya.

*Wapelelezi Wanatumwa*

**(Hesabu 13:1-33)**

19 [b]Kisha, kama Bwana Mungu wetu
alivyotuamuru, tuliondoka kutoka Horebu
na kwenda kuelekea nchi ya vilima ya
Waamori, kupitia jangwa lile kubwa lote
la kutisha, lile mlililoliona, nasi tukafika
Kadesh-Barnea. 20 Kisha niliwaambia,
"Mmefika katika nchi ya vilima ya Waamori,
ambayo Bwana Mungu wetu anatupa.
21 [c]Tazama, Bwana Mungu wenu amewapa
nchi. Pandeni mkaimiliki kama Bwana,
Mungu wa baba zenu, alivyowaambia.
Msiogope, wala msikate tamaa."

22 [d]Ndipo ninyi nyote mkanijia na
kusema, "Tupeleke watu watutangulie
kuipeleleza nchi kwa ajili yetu, na kutuletea
taarifa kuhusu njia tutakayopita, na miji
tutakayoiendea."

23 [e]Wazo hilo lilionekana zuri kwangu;
kwa hiyo niliwachagua watu wenu kumi
na wawili, mwanaume mmoja kutoka kila
kabila. 24 [f]Waliondoka na kukwea katika
nchi ya vilima, wakafika katika Bonde la
Eshkoli na kuipeleleza. 25 [g]Wakachukua
baadhi ya matunda ya nchi, wakatuletea na
kutuarifu, "Ni nchi nzuri ambayo Bwana
Mungu wetu anatupa."

*Uasi Dhidi Ya Bwana*

**(Hesabu 14:20-45)**

26 [h]Lakini hamkuwa tayari kukwea,
mkaasi dhidi ya amri ya Bwana Mungu
wenu. 27 [i]Mkanung'unika ndani ya mahema
yenu na kusema, "Bwana anatuchukia,
kwa hiyo alitutoa Misri ili kututia mikononi
mwa Waamori kutuangamiza. 28 [j]Twende
wapi? Ndugu zetu wametufanya kufa moyo.
Wanasema, 'Watu wa huko wana nguvu
zaidi na ni warefu kuliko sisi tulivyo; miji ni
mikubwa, yenye kuta zilizofika juu angani.
Zaidi ya hayo, tumewaona Waanaki huko.' "

29 [k]Ndipo nikawaambia, "Msihofu, wala
msiwaogope. 30 [l]Bwana Mungu wenu
anayewatangulia, atawapigania, kama
alivyofanya kwa ajili yenu huko Misri,
mbele ya macho yenu hasa, 31 [m]na pia
huko jangwani. Huko mliona jinsi Bwana
Mungu wenu alivyowachukua, kama baba
amchukuavyo mwanawe, katika njia yote
mliyoiendea mpaka mkafika mahali hapa."

32 [n]Pamoja na hili, hamkumtegemea
Bwana Mungu wenu, 33 [o]ambaye
aliwatangulia katika safari yenu, kwa
moto usiku na kwa wingu mchana,
kuwatafutia mahali penu pa kupiga kambi
na kuwaonyesha njia mtakayoiendea.

34 [p]Wakati Bwana aliposikia lile
mlilosema, alikasirika, akaapa, akasema:
35 [q]"Hakuna mtu wa kizazi hiki kiovu
atakayeona nchi nzuri niliyoapa kuwapa
baba zenu, 36 [r]isipokuwa Kalebu mwana
wa Yefune. Yeye ataiona, nami nitampa
yeye na wazao wake nchi aliyoikanyaga
kwa miguu, kwa sababu alimfuata Bwana
kwa moyo wote."

37 [s]Kwa sababu yenu Bwana pia

---

[a]**1:18** Mwa 39:11
[b]**1:19** Kum 2:7; 8:15; 32:10; Za 136:16; Yer 2:2-6; Hos 13:5; Hes 13:26
[c]**1:21** Kum 29:23; Hes 14:9; Yos 1:6-9, 18; 2Sam 10:12; Za 27:14; Kum 7:18; Yos 8:1; 10:8
[d]**1:22** Hes 13:1-3; Mwa 42:9
[e]**1:23** Hes 13:1-3
[f]**1:24** Hes 13:21-25; 32:9
[g]**1:25** Hes 13:27; 14:7; Yos 1:2
[h]**1:26** Hes 14:1-4; 14:9; Za 106:24
[i]**1:27** Kum 9:28; Za 106:25
[j]**1:28** Hes 13:32-33; Kum 9:1-3
[k]**1:29** Kum 3:22; 20:3; Neh 4:14; Kum 7:18; 20:1; 31:6
[l]**1:30** Kut 14:14; Neh 4:20
[m]**1:31** Kut 19:4; Kum 32:10-12; Za 28:9; Isa 46:3-4; 63:9; Hos 11:3; Mdo 13:18; Yer 31:32
[n]**1:32** Hes 14:11; Kum 9:23; Za 78:22; 106:24; Sef 3:2; Ebr 3:19; Yud 5
[o]**1:33** Kut 13:21; Hes 9:15-23; Neh 9:12; 9:12; Za 78:14; Hes 10:33
[p]**1:34** Hes 11:1; 32:14; 14:23; 28:30; Eze 20:15; Ebr 3:11
[q]**1:35** Hes 14:29; 14:22; Za 95:11
[r]**1:36** Hes 13:6; 14:24
[s]**1:37** Za 106:32; Hes 27:13, 14; Kum 3:26; 4:21; 34:4

alinikasirikia mimi, akasema, “Hutaingia
hiyo nchi pia. 38 [a]Lakini msaidizi wako,
Yoshua mwana wa Nuni, ataingia. Mtie
moyo, kwa sababu atawaongoza Waisraeli
kuirithi hiyo nchi. 39 [b]Wale watoto ambao
mliwasema wangelichukuliwa mateka,
yaani watoto wenu ambao bado hawajui
jema na baya, wataingia katika nchi.
Nitawapa hiyo nchi, nao wataimiliki.
40 [c]Bali ninyi geukeni, mwondoke kuelekea
jangwani kwa kufuata njia ya Bahari ya
Shamu.”

41 Ndipo mkanijibu, “Tumemtenda
Bwana dhambi. Tutakwenda kupigana,
kama Bwana Mungu wetu alivyotuamuru.”
Hivyo kila mmoja wenu akachukua silaha
zake, huku mkifikiri kuwa ni rahisi kukwea
katika nchi ya vilima.

42 [d]Lakini Bwana aliniambia, “Waambie,
‘Msipande kupigana, kwa sababu sitakuwa
pamoja nanyi. Mtashindwa na adui zenu.’ ”

43 [e]Hivyo niliwaambia, lakini hamkutaka
kusikia. Mliasi dhidi ya amri ya Bwana,
na katika kiburi chenu mlienda katika
nchi ya vilima. 44 [f]Waamori ambao
waliishi katika vilima hivyo waliinuka
dhidi yenu, wakawafukuza kama kundi
la nyuki wakiwapiga njia yote ya Seiri
mpaka Horma. 45 [g]Mlirudi na kulia mbele
za Bwana, lakini Mungu hakusikiliza kilio
chenu, wala hakuwajali. 46 [h]Hivyo mlikaa
Kadeshi kwa siku nyingi, kwa muda ule
wote mliokaa huko.

### *Kutangatanga Jangwani*

2 [i]Kisha tukageuka nyuma na
kusafiri kuelekea jangwani kwa njia
inayoelekea Bahari ya Shamu, kama
Bwana alivyonielekeza. Kwa muda mrefu
tulitembea kuzunguka vilima katika nchi
ya Seiri.

2 Kisha Bwana akaniambia,
3 [j]“Umetembea kuzunguka hii nchi ya
vilima kwa muda wa kutosha; sasa geukia
kaskazini. 4 [k]Wape watu maagizo haya:
‘Mko karibu kupita katikati ya nchi ya
ndugu zako ambao ni wazao wa Esau,
ambao wanaishi Seiri. Watawaogopa,
lakini mwe waangalifu. 5 [l]Msiwachokoze
kwa vita kwa maana sitawapa ninyi sehemu
yoyote ya nchi yao, hata sehemu ya kutosha
kuweka wayo wenu juu yake. Nimempa
Esau nchi ya vilima ya Seiri kama yake
mwenyewe. 6 Mtawalipa fedha kwa chakula
mtakachokula na maji mtakayokunywa.’ ”

7 [m]Bwana Mungu wenu amewabariki
kwa kazi yote ya mikono yenu. Amewalinda
katika safari yenu katikati ya jangwa hili
kubwa. Kwa miaka hii arobaini Bwana
Mungu wenu amekuwa pamoja nanyi, na
hamkupungukiwa na kitu chochote.

8 [n]Basi tulipita kwa ndugu zetu wazao
wa Esau ambao wanaishi Seiri. Tuligeuka
kutoka njia ya Araba ambayo inatokea
Elathi na Esion-Geberi, tukasafiri kufuata
njia ya jangwa la Moabu.

9 [o]Kisha Bwana akaniambia,
“Usiwasumbue Wamoabu kwa vita, kwa
kuwa sitawapa sehemu yoyote ya nchi yao.
Nimetoa nchi ya Ari kwa wazao wa Loti
kama milki yao.”

10 [p](Waemi walikuwa wakiishi huko
hapo zamani, watu wenye nguvu na
wengi, warefu kama Waanaki. 11 [q]Kama
walivyokuwa Waanaki, hao pia walikuwa
kama Warefai, lakini Wamoabu waliwaita
Waemi. 12 [r]Wahori waliishi Seiri,

[a]**1:38** Hes 11:28; Kum 31:7; 3:28; Yos 11:23; Za 78:55; 136:21
[b]**1:39** Hes 14:3; Isa 7:15-16
[c]**1:40** Kut 14:27; Amu 11:16
[d]**1:42** Hes 14:41-43
[e]**1:43** Hes 14:44
[f]**1:44** Za 118:12; Hes 28:18; 14:45; Kum 28:25; 32:30; Isa 7:18
[g]**1:45** Hes 14:1; Ay 27:9; 35:13; Za 18:41; 66:18; Mit 1:28; Isa 1:15; Yer 14:12; Mao 3:8; Mik 3:4; Yn 9:31; Za 28:1; 39:12; Mit 28:9
[h]**1:46** Hes 20:1; 13:25; Amu 11:27
[i]**2:1** Kut 14:27; Hes 21:4; 24:18
[j]**2:3** Kum 1:6
[k]**2:4** Hes 20:14-21; Mwa 36:8; Kut 15:16
[l]**2:5** Yos 24:4; Mwa 36:8; Kum 32:8; 2Nya 20:10-12; Mdo 17:26
[m]**2:7** Kum 8:2-4; Kut 13:21; Kum 1:19; Hes 14:33; 32:13; Yos 5:6; Neh 9:21; Amo 2:10
[n]**2:8** Hes 20:8; 33:35; 1Fal 9:26; Hes 21:4
[o]**2:9** Hes 21:15; Mwa 19:38; Za 83:8
[p]**2:10** Mwa 14:5; Hes 13:22; 33; Kum 9:2
[q]**2:11** Mwa 14:5
[r]**2:12** Mwa 14:6; Hes 21:25-35

lakini wazao wa Esau waliwafukuza.
Waliwaangamiza Wahori na kukaa mahali
pao, kama Waisraeli walivyofanya katika
nchi ambayo BWANA aliwapa kama milki
yao.)
13 [a]BWANA akasema, "Sasa ondokeni
mvuke Bonde la Zeredi." Hivyo tukavuka
bonde.
14 [b]Miaka thelathini na minane ilipita
tangu wakati tulipoondoka Kadesh-
Barnea mpaka tulipovuka Bonde la Zeredi.
Kwa wakati huo kile kizazi chote cha
wanaume kuanzia wale wawezao kwenda
vitani kilikuwa kimekufa, kama BWANA
alivyokuwa amewaapia. 15 [c]Mkono wa
BWANA uliwakabili hadi alipowaangamiza
wote huko kambini.
16 Ikawa baada ya mtu wa mwisho
kuanzia wale wawezao kwenda vitani
kufa, 17 BWANA akaniambia, 18 [d]"Leo
utapita katika nchi ya Moabu huko
Ari. 19 [e]Utakapokuja kwa Waamoni,
msiwasumbue wala kuwachokoza kwa vita,
kwa kuwa sitawapa ardhi yoyote iliyo ya
Waamoni kuwa milki yenu. Nimeitoa kama
milki ya wazao wa Loti."
20 [f](Hiyo pia ilidhaniwa kuwa nchi
ya Warefai waliokuwa wakiishi huko,
lakini Waamoni waliwaita Wazamzumi.
21 Walikuwa watu wenye nguvu na
wengi, warefu kama Waanaki. BWANA
akawaangamiza kutoka mbele ya Waamoni,
ambao waliwafukuza na kukaa mahali pao.
22 [g]BWANA alikuwa amefanya vivyo hivyo
kwa wazao wa Esau, ambao waliishi Seiri,
wakati alipowaangamiza Wahori watoke
mbele yao. Waliwafukuza na wao wakaishi
mahali pao mpaka leo. 23 [h]Nao Waavi ambao
waliishi katika vijiji mpaka Gaza, Wakaftori
waliokuja kutoka Kaftori waliwaangamiza
na kukaa mahali pao.)
24 [i]"Ondoka sasa na uvuke Bonde la
Arnoni. Tazama, nimemweka mikononi
mwako Sihoni Mwamori, mfalme wa
Heshboni na nchi yake. Anza kuimiliki nchi
hiyo na umwingize katika vita. 25 [j]Siku hii ya
leo nitaanza kuwatia hofu na woga mataifa
yote chini ya mbingu wawaogope ninyi.
Watakaposikia taarifa zenu, watatetemeka
na kufadhaika kwa sababu yenu."

*Kushindwa Kwa Sihoni Mfalme Wa Heshboni*

**(Hesabu 21:21-30)**

26 [k]Kutoka jangwa la Kedemothi nilituma
wajumbe wenye maneno ya amani kwa
Sihoni mfalme wa Heshboni kusema,
27 [l]"Turuhusu tupite katika nchi yako.
Tutapita katika barabara kuu, hatutageuka
kuume wala kushoto. 28 [m]Tuuzie chakula
tule na maji tunywe kwa thamani yake
katika fedha. Turuhusu tu tupite kwa miguu,
29 [n]kama wazao wa Esau ambao wanaishi
Seiri na Wamoabu ambao wanaishi Ari
walivyotufanyia, mpaka tuvuke Yordani
kuingia nchi ambayo BWANA Mungu wetu
anatupatia." 30 [o]Lakini Sihoni mfalme wa
Heshboni alikataa kuturuhusu kupita.
Kwa kuwa BWANA Mungu wako alikuwa
ameifanya roho yake kuwa ngumu na moyo
wake kuwa mkaidi ili amweke kwenye
mikono yenu, kama alivyofanya sasa.
31 [p]BWANA akaniambia, "Tazama,
nimeanza kuwapa Mfalme Sihoni na nchi
yake kwako. Sasa anzeni kuishinda na
kuimiliki nchi yake."

---

[a]**2:13** Hes 21:12
[b]**2:14** Kum 1:2; Hes 13:26; 14:29-35; Kum 1:34-35; Yos 5:6
[c]**2:15** Za 106:26; Yud 5; 1Sam 5:6-11; 7:13; Za 95:10, 11; Ebr 4:1-5
[d]**2:18** Hes 21:15
[e]**2:19** Mwa 19:38; 2Nya 20:10
[f]**2:20** Mwa 14:5
[g]**2:22** Mwa 14:6; 36:8; Ay 12:23
[h]**2:23** Yos 13:3; 18:23; 2Fal 17:31; Mwa 10:14; 19; Yer 47:4; Amo 9:7; Sef 2:4
[i]**2:24** Hes 21:13-14; Amu 11:13-18; Kum 1:7; 3:6
[j]**2:25** Mwa 35:5; Kum 1:25; Yos 2:9-11; 1Nya 14:17; 2Nya 14:14; 17:10; 20:29; Isa 2:19; 13:13; 19:16; Kut 15:14-16
[k]**2:26** Yos 13:18; 1Nya 6:79; Kum 1:4; Amu 1:11-22; Kum 20:10; Amu 21:13; 2Sam 20:19
[l]**2:27** Hes 21:21-22; Amu 11:19
[m]**2:28** Kum 23:4; Hes 20:19
[n]**2:29** Kum 23:3; Amu 11:17
[o]**2:30** Amu 14:4; 1Fal 12:15; Kut 4:21; Rum 9:18; Kut 14:17; Yos 11:20; Hes 21:23; Mao 3:65; Yos 11:19, 20; Hos 4:17; Yak 1:13-15
[p]**2:31** Mwa 12:7; Kum 1:8

32 [a]Wakati Sihoni pamoja na jeshi lake lote walipokuja kukutana nasi katika vita huko Yahazi, 33 [b]BWANA Mungu wetu alimweka mikononi mwetu, nasi tukamwangamiza pamoja na wanawe na jeshi lake lote. 34 [c]Kwa wakati ule tuliteka miji yake yote na kuiangamiza kabisa: wanaume, wanawake na watoto. Hatukumwacha yeyote. 35 [d]Lakini mifugo na nyara tulizoziteka kutoka ile miji tulijichukulia wenyewe. 36 [e]Kutoka Aroeri kwenye ukingo wa Bonde la Arnoni, kutoka mji ulio ndani ya bonde, hata mpaka Gileadi, hapakuwa na mji hata mmoja uliokuwa na nguvu kutushinda. BWANA Mungu wetu alitupa yote. 37 [f]Lakini kulingana na amri ya BWANA Mungu wetu, hamkujiingiza katika nchi yoyote ya Waamoni, wala katika sehemu yoyote iliyo kandokando ya Mto Yaboki, wala katika miji iliyoko katika vilima.

*Kushindwa Kwa Ogu Mfalme Wa Bashani*

**(Hesabu 21:31-35)**

3 [g]Kisha tukageuka tukakwea kufuata njia iliyoelekea Bashani, Ogu mfalme wa Bashani akaondoka na jeshi lake lote kupigana na sisi huko Edrei. 2 [h]BWANA akaniambia, “Usimwogope kwa kuwa nimekwisha mkabidhi mikononi mwako pamoja na jeshi lake lote na nchi yake. Umfanyie sawasawa na ulivyomfanyia Sihoni mfalme wa Waamori, ambaye alitawala huko Heshboni.”

3 [i]Hivyo BWANA Mungu wetu pia akamweka Ogu mfalme wa Bashani pamoja na jeshi lake lote mikononi mwetu. Tuliwaangamiza wote, hakubakia hata mmoja. 4 [j]Wakati huo tuliteka miji yake yote. Hakuna mji hata mmoja kati ya ile sitini ambao hatukuuteka, yaani eneo lote la Argobu, utawala wa Mfalme Ogu katika Bashani. 5 Miji yote hii ilijengewa ngome zenye kuta ndefu zenye malango na makomeo, pia kulikuwako na vijiji vingi ambavyo havikujengewa kuta. 6 [k]Tuliwaangamiza kabisa, kama tulivyomfanyia Sihoni mfalme wa Heshboni, tukiangamiza kila mji, yaani wanaume, wanawake na watoto. 7 [l]Lakini wanyama wote wa kufuga pamoja na nyara kutoka kwenye miji yao tulichukua vikawa vyetu.

8 [m]Hivyo kwa wakati huo tukachukua kutoka kwa wafalme hawa wawili wa Waamori nchi ya mashariki ya Yordani, kutoka Bonde la Arnoni mpaka kufika kwenye Mlima Hermoni. 9 [n](Wasidoni huuita mlima huo Sirioni, nao Waamori huuita Seniri.) 10 [o]Tuliteka miji yote kwenye uwanda wa juu, Gileadi yote, Bashani yote mpaka kufika Saleka na Edrei, miji ya utawala wa Ogu huko Bashani. 11 [p](Mfalme Ogu wa Bashani ndiye peke yake aliyesalia miongoni mwa mabaki ya Warefai. Kitanda chake kilikuwa cha chuma chenye urefu wa dhiraa tisa[q] na upana wa dhiraa nne.[r] Mpaka sasa kinaweza kuonekana katika mji wa Waamoni wa Raba.)

*Mgawanyo Wa Nchi Mashariki Ya Yordani*

**(Hesabu 32:1-42)**

12 [s]Katika nchi tuliyoiteka wakati ule, niliwapa kabila la Reubeni na Gadi eneo lililoko kaskazini la Aroeri kando ya Bonde

---

[a]**2:32** Hes 21:23
[b]**2:33** Kut 23:31; Kum 7:2; 31:5; 29:7; Hes 21:24; Za 135:10-12; 136:18-20
[c]**2:34** Hes 21:2; Kum 3:6; 7:2; Za 106:34; Law 27:28; Kum 7:2, 26; Yos 7:11; 8:25, 26; 9:24; 11:14; 1Sam 15:3-9
[d]**2:35** Kum 3:7; Mwa 34:29; 49:27
[e]**2:36** Hes 32:34; 32:39; Za 44:3; Yos 13:9
[f]**2:37** Hes 21:21; Mwa 32:22; Kum 3:16
[g]**3:1** Hes 21:33; 32:19
[h]**3:2** Yos 10:8; 2Fal 19:6; Isa 7:4
[i]**3:3** Hes 21:24; 21:35
[j]**3:4** Hes 21:24, 33; 1Fal 4:13
[k]**3:6** Kum 2:24; Za 135:10-12; 136:19-21
[l]**3:7** Kum 2:35
[m]**3:8** Hes 32:33; Yos 13:8-12; Kum 4:48; Yos 11:3; 12:1; 13:5; Amu 3:3; 1Nya 5:23; Za 42:6; 89:12; 133:3; Wim 4:8
[n]**3:9** Za 29:6; 89:12; 1Nya 5:23; Wim 4:8; Eze 27:5; Kum 4:48
[o]**3:10** Yos 12:5; 13:11; 1Nya 5:11; Kum 4:49
[p]**3:11** Mwa 14:5; Yos 13:25; 15:60; 2Sam 11:1; 12:26; 17:27; 1Nya 20:7; Yer 49:2; Eze 21:20; 25:5; Amo 1:14; 2:9
[q]11 Dhiraa tisa ni sawa na mita 4.
[r]11 Dhiraa nne ni sawa na mita 1.8.
[s]**3:12** Kum 2:36; Hes 32:32-38; Yos 13:8-13

la Arnoni, na nusu ya eneo la milima ya
Gileadi, pamoja na miji yake. [13] [a]Kisha nusu
ya kabila la Manase niliwapa sehemu ya
Gileadi iliyobaki pamoja na Bashani yote,
ambayo ilikuwa utawala wa Ogu. (Eneo
lote la Argobu katika Bashani lilikuwa
linajulikana kama nchi ya Warefai. [14] [b]Yairi,
mzao wa kabila la Manase, alichukua eneo
lote la nchi ya Argobu hadi kufikia mpaka
wa Wageshuri na Wamaaka, ukaitwa kwa
jina lake; kwa hiyo mpaka leo hii Bashani
inaitwa Hawoth-Yairi.) [15] [c]Nikampa
Makiri nchi ya Gileadi. [16] [d]Lakini niliwapa
Wareubeni na Wagadi eneo kuanzia Gileadi
hadi Bonde la Arnoni (katikati ya bonde
ulikuwa ndio mpaka), kuelekea mpaka Mto
Yaboki, ambao ndio mpaka wa Waamoni.
[17] [e]Kwa upande wa magharibi mpaka wao
ulikuwa Yordani katika Araba, toka ziwa
Galilaya hadi Bahari ya Araba (yaani Bahari
ya Chumvi), kwenye miteremko ya Pisga
upande wa mashariki.

[18] [f]Wakati huo nilikuamuru: "BWANA
Mungu wako amekupa nchi hii uimiliki.
Lakini ni lazima wanaume wenu wote
wenye uwezo, wakiwa wamejiandaa tayari
kwa vita, wavuke ng'ambo wakiwatangulia
ndugu zako Waisraeli. [19] [g]Lakini wake
zenu, watoto wenu na mifugo yenu (kwani
najua mnayo mifugo mingi) wanaweza
kukaa katika miji niliyowapa, [20] [h]mpaka
hapo BWANA atakapowapa ndugu zenu
kupumzika kama alivyowapa ninyi, wao pia
wamiliki ile nchi ambayo BWANA Mungu
wenu anawapa, ng'ambo ya Yordani. Baada
ya hapo, kila mmoja wenu anaweza kurudi
kwenye milki niliyowapa."

*Mose Akatazwa Kuvuka Yordani*

[21] Wakati huo nilimwamuru Yoshua,
"Umejionea kwa macho yako mwenyewe
yale yote ambayo BWANA Mungu wenu
amewafanyia wafalme hawa wawili. BWANA
atazifanyia falme zote huko mnakokwenda
vivyo hivyo. [22] [ij]Msiwaogope, BWANA
Mungu wenu atapigana kwa ajili yenu."

[23] [k]Wakati huo nilimsihi BWANA: [24] [l]"Ee
BWANA Mwenyezi, umemwonyesha
mtumishi wako ukuu wako na mkono
wako wenye uweza. Kwa kuwa ni mungu
yupi aliye mbinguni au duniani anayeweza
kufanya kazi na matendo makuu kama
ufanyayo wewe? [25] [m]Acha niende nikaione
hiyo nchi nzuri ng'ambo ya Yordani, ile
nchi nzuri ya vilima na Lebanoni."

[26] [n]Lakini kwa sababu yenu BWANA
alinikasirikia na hakutaka kunisikiliza.
BWANA aliniambia, "Hilo latosha; usiseme
nami jambo hili tena. [27] [o]Kwea juu ya kilele
cha Pisga uangalie magharibi, kaskazini,
kusini na mashariki. Iangalie hiyo nchi
kwa macho yako, kwa vile wewe hutavuka
Yordani. [28] [p]Lakini mwagize Yoshua, mtie
moyo na umtie nguvu, kwa kuwa yeye
atawaongoza watu hawa hadi ng'ambo na
kuwarithisha nchi utakayoiona." [29] [q]Kwa
hiyo tulikaa kwenye bonde karibu na
Beth-Peori.

*Waamriwa Utii*

4 [r]Sikia sasa, ee Israeli, amri na sheria
nitakazokufundisha wewe. Zifuate
ili upate kuishi na uingie kuimiliki nchi

---

[a]**3:13** Kum 29:8; Mwa 14:5
[b]**3:14** Hes 32:41; Yos 12:5; 13:11-13; 2Sam 10:6; 23:34; 2Fal 25:23; 1Nya 4:19; Yer 40:8; Yos 19:46-47; Za 49:11; 1Nya 2:22
[c]**3:15** Mwa 50:23; Hes 32:39-40
[d]**3:16** Hes 21:24; 2Sam 24:5; Hes 21:24
[e]**3:17** 2Sam 2:29; 4:7; Eze 47:8; Hes 34:11; 14:3; Yos 12:3; 13:27
[f]**3:18** Yos 1:13; Hes 32:17
[g]**3:19** Yos 1:14; Hes 32:16
[h]**3:20** Yos 22:4
[i]**3:22** Kum 1:29; 7:18; 20:4; 31:6; 2Nya 32:8; Za 23:4; Isa 41:10; Kut 14:14
[j]**3:22** Yos 23:10
[k]**3:23** Kum 1:37; 31:2; 32:52; 34:4
[l]**3:24** Kum 5:24; 11:2; 32:3; Kut 8:10; Za 71:16; 86:8; 106:2; 145:12; 150:2; 2Sam 7:22; Neh 9:32; Yer 32:18-21; Kut 15:11
[m]**3:25** Kum 4:25; 1:7; Yos 1:4; 9:1; 11:17; 12:7; 13:5; Amu 3:3; 9:13; 1Fal 4:33
[n]**3:26** Kum 1:37; 31:2
[o]**3:27** Hes 21:20; 27:12; Mwa 13:14; Hes 20:12; Kum 32:52
[p]**3:28** Hes 27:18-23; Kum 31:7; 1:38; 31:3-23
[q]**3:29** Hes 23:28; Kum 4:46; 34:6; Yos 13:20
[r]**4:1** Law 18:4-5; Kum 1:3; 30:15-20; Rum 10:5; Eze 20:11; Rum 10:5

ambayo BWANA, Mungu wa baba zako
anawapa. 2 [a]Usiongeze wala usipunguze
chochote ninachowaamuru ninyi, ila
myashike maagizo ya BWANA Mungu wenu
ambayo nawapa.
3 [b]Mliona kwa macho yenu wenyewe
kile BWANA alichokifanya kule Baal-Peori.
BWANA Mungu wenu aliwaangamiza
kutoka miongoni mwenu kila mmoja
aliyemfuata Baali wa Peori, 4 lakini ninyi
nyote mlioshikamana na BWANA kwa
uthabiti, Mungu wenu, mko hai mpaka leo.
5 [c]Tazama, nimewafundisha amri na
sheria kama BWANA Mungu wangu
alivyoniamuru mimi, ili mzifuate katika
nchi mnayoiingia kuimiliki. 6 [d]Zishikeni
kwa uangalifu, kwa kuwa hii itaonyesha
hekima na ufahamu wenu kwa mataifa,
ambayo yatasikia kuhusu amri zote hizi,
nao watasema, "Hakika taifa hili kubwa
ni watu wenye hekima na ufahamu." 7 [e]Ni
taifa gani jingine lililo kubwa kiasi cha
kuwa na miungu yao iliyo karibu nao kama
BWANA Mungu wetu alivyo karibu nasi
wakati wowote tunapomwomba? 8 [f]Nalo
ni taifa gani jingine lililo kubwa hivi lenye
kuwa na amri na sheria za haki kama hizi
ninazoweka mbele yenu leo?
9 [g]Mwe waangalifu, na makini ili msije
mkasahau mambo ambayo mliyaona kwa
macho yenu, wala kuyaacha yaondoke
moyoni mwenu siku zote za uhai wenu.
Mwafundishe hayo watoto wenu na watoto
wao baada yao.
10 [h]Kumbuka siku uliyosimama mbele za
BWANA Mungu wako kule Horebu, wakati
aliponiambia, "Wakutanishe watu mbele
yangu wasikie maneno yangu ili kwamba
waweze kujifunza kuniheshimu kwa muda
wote watakaoishi katika nchi, nao waweze
kuwafundisha watoto wao maneno hayo."
11 [i]Mlisogea karibu na mkasimama chini
ya mlima wakati ulipowaka moto mpaka
mbinguni juu, pamoja na mawingu meusi na
giza nene. 12 [j]Ndipo BWANA alipozungumza
nanyi kutoka moto. Mkasikia sauti ya
maneno lakini hamkuona umbo, kulikuwa
na sauti tu. 13 [k]Aliwatangazia Agano lake na
Amri Kumi, ambazo aliwaamuru mzifuate,
kisha akaziandika juu ya vibao viwili vya
mawe. 14 Naye BWANA alinielekeza wakati
huo kuwafundisha ninyi sheria na amri
ambazo mnapaswa kuzifuata katika nchi
ambayo mnavuka Yordani kuimiliki.

*Kuabudu Sanamu Kwakatazwa*

15 [l]Hamkuona umbo la aina yoyote siku
ambayo BWANA alizungumza nanyi kule
Horebu kutoka kwenye moto. Kwa hiyo
mjihadhari kwa uangalifu sana, 16 [m]ili
msije mkajichafua na kujitengenezea
sanamu au kinyago chenye umbo lolote
kama la mwanaume au mwanamke, 17 [n]au
kama mnyama aliye juu ya nchi au ndege
yeyote arukaye angani, 18 au kama kiumbe
kitambaacho juu ya ardhi au samaki yeyote

---

[a]**4:2** Kum 12:32; Yos 1:7; Mit 30:6; Ufu 22:18-19; Yer 26:2; Law 22:31; Kum 10:12-13; Mhu 12:13
[b]**4:3** Hes 25:1-9; Za 106:28
[c]**4:5** Za 71:17; 119:102; Yer 32:33; Kut 18:20; Law 27:34; Ezr 9:11
[d]**4:6** Kum 29:9; 1Fal 2:3; Kum 30:19-20; 32:46-47; Za 19:7; 119:98; Mit 1:7; 2:5; 2Tim 3:15; Ay 28:28; Za 111:10; Mit 3:7; 9:10; Mhu 12:13; Eze 5:5
[e]**4:7** 2Sam 7:23; Hes 23:21; Za 46:1; Mdo 17:27; Kut 25:8; 29:45; Law 26:12; 1Fal 6:13; Isa 55:6; Zek 2:10; Efe 2:17; Yak 4:8
[f]**4:8** Za 89:14; 97:2; 119:7, 62, 144, 160, 172; Rum 3:2
[g]**4:9** Kut 23:13; Mwa 14:14; 18:19; Kum 6:20-25; Efe 6:4; Kut 10:2; Mit 4:23; Za 78:5-6; Mit 4:23; 23:19; 3:1, 3; 4:21; Mwa 18:19; Mit 22:6; Efe 6:4
[h]**4:10** Kut 3:1; 19:9, 16; Kum 14:23; 17:19; 31:12-13; Za 2:11; 111:10; 147:11; Isa 8:13; Yer 32:40; Kut 20:20; Kum 12:1
[i]**4:11** Kut 3:1; 19:17-18; 19:9; Za 18:11; 97:2; Ebr 12:18-19
[j]**4:12** Kut 20:22; Mt 3:17; Kum 5:4-20; Ebr 12:19; Yn 5:37; Kut 19:9
[k]**4:13** Kum 9:9-11; Rum 9:4; Kut 24:12; 31:18; 4:14; 21:1
[l]**4:15** Isa 40:18; 41:22-24; Kut 3:1; Yos 23:11; Mal 2:15; Mit 4:23, 27; Yer 17:21; Mdo 17:24-29
[m]**4:16** Mwa 6:11-12; Kum 9:12; 31:29; 32:5; Amu 2:19; Kut 20:4-5; 32:7; Rum 1:23
[n]**4:17** Rum 1:23

aliye ndani ya maji. [19] [a]Na utazamapo juu
angani na ukaliona jua, mwezi na nyota
na vyote vinavyoipamba mbingu, usije
ukashawishiwa kuviinamia na kuviabudu
vile ambavyo BWANA Mungu wenu
alivyogawia mataifa yote chini ya mbingu.
[20] [b]Lakini kwenu ninyi, BWANA amewatoa
kutoka kwenye tanuru ya kuyeyushia
chuma, katika Misri kuwa watu wa urithi
wake kama mlivyo sasa.

[21] [c]BWANA alinikasirikia kwa sababu yenu
na akaapa kwamba sitavuka Yordani kuingia
katika nchi nzuri BWANA Mungu wenu
anayowapa kuwa urithi wenu. [22] [d]Nitakufa
katika nchi hii; sitavuka Yordani, lakini
ninyi ni karibu mvuke mkaimiliki ile nchi
nzuri. [23] [e]Jihadharini msilisahau Agano la
BWANA Mungu wenu lile alilofanya nanyi;
msijitengenezee sanamu katika umbo la
kitu chochote ambacho BWANA Mungu
wenu amewakataza. [24] [f]Kwa kuwa BWANA
Mungu wenu ni moto ulao, Mungu mwenye
wivu.

[25] [g]Baada ya kuwa na watoto na wajukuu
na kuishi katika nchi hiyo siku nyingi, tena
kama mkijichafua na kutengeneza sanamu
ya aina yoyote, mkifanya maovu machoni
pa BWANA Mungu wenu na kumfanya awe
na hasira, [26] [h]ninaziita mbingu na nchi kama
mashahidi dhidi yenu siku hii kwamba
mtaangamia mara moja kutoka nchi ile
ambayo mnavuka Yordani kuimiliki.
Hamtaishi kule kwa muda mrefu bali
kwa hakika mtaangamizwa. [27] [i]BWANA
atawatawanya miongoni mwa mataifa,
na ni wachache wenu tu watakaosalia
miongoni mwa mataifa hayo ambayo
BWANA atawafukuzia. [28] [j]Huko mtaabudu
miungu ya miti na mawe iliyotengenezwa
na watu, ambayo haiwezi kuona au
kusikia wala kula au kunusa. [29] [k]Lakini
kama mtamtafuta BWANA Mungu wenu,
mtampata; kama mtamtafuta kwa moyo
wenu wote na kwa roho yote. [30] [l]Wakati
mnapokuwa katika dhiki, nayo mambo
haya yote yamewatokea siku hizo, ndipo
mtamrudia BWANA Mungu wenu na kumtii.
[31] [m]Kwa maana BWANA Mungu wenu ni
Mungu mwenye huruma, hatawaacha
au kuwaangamiza wala kusahau Agano
alilofanya na baba zenu, alilowathibitishia
kwa kiapo.

### *BWANA Ndiye Mungu*

[32] [n]Sasa uliza kuhusu siku za zamani,
zamani kabla ya wakati wako, tangu siku
ile Mungu alipomuumba mtu juu ya nchi,
uliza kutoka mwisho mmoja wa mbingu
mpaka mwisho mwingine wa mbingu.
Je, kumepata kutokea jambo jingine lililo
kubwa kama hili, au kuna jambo jingine
kama hilo limepata kusikiwa? [33] [o]Je, kuna
watu wengine wowote waliosikia sauti
ya Mungu ikizungumza kwenye moto,

---

[a]**4:19** 2Fal 23:11; Kum 17:3; Ay 31:26; Yer 8:2; 43:13; Eze 8:16; Mwa 1:16; 2:1; 37:9; Rum 1:25; Kum 13:5; Hes 25:3

[b]**4:20** Kut 1:13; 3:10; Mwa 17:7; Kut 8:22; 34:9; Tit 2:14; Kut 19:5

[c]**4:21** Hes 20:12; Kum 1:37

[d]**4:22** Hes 27:13-14; Kum 3:25

[e]**4:23** Kut 20:4

[f]**4:24** Kut 15:7; 19:18; Ebr 12:29; Kut 20:5

[g]**4:25** 1Fal 11:6; 15:26; 16:25-30; 2Fal 17:2; 17:21

[h]**4:26** Mwa 31:50; Mit 14:5; Kum 30:18-19; 31:28; 32:1; Za 50:4; Isa 1:2; 34:1; Yer 6:19; Mik 6:2; Kum 6:15; 7:4

[i]**4:27** Law 26:23; Kum 28:36-64; 29:28; 1Fal 8:46; 2Fal 17:16; Za 44:11; 106:27; Yer 3:8; Mik 1:16; Isa 17:6; 21:17; Oba 1:5; Neh 1:8

[j]**4:28** Kum 13:2; 28:36-64; 1Sam 26:19; Yer 5:19; 16:13; Mdo 19:26; Kum 29:17; Za 115:4-8; 135:15-18; Isa 8:19; 26:14; 44:17-20; Ufu 9:20

[k]**4:29** 1Sam 13:12; 2Fal 13:4; 2Nya 7:14; 15:4; 33:12; Za 78:34; 119:58; Isa 45:19, 22; 55:6; Yer 26:19; Dan 9:13; Hos 3:5; Amo 5:4; 1Sam 7:3; 1Fal 8:48; Yer 29:13; Kum 6:5; 30:1-3, 10

[l]**4:30** Hos 3:5; Law 26:41; Kum 31:17-21; Za 4:1; 18:6; 48:1; 59:16; 107:6; Kum 31:29; Yer 23:20; 3:1-12, 22; 4:1; 18:11; Ebr 1:2; Kum 30:2; 1Fal 8:48; Neh 1:9; Yoe 2:12

[m]**4:31** Kut 34:6; Neh 9:31; Za 111:9; Kum 31:6-8; Yoe 1:5; 1Fal 8:57; 1Nya 28:9-20; Za 9:10; 27:9; 71:9; Isa 42:16; Ebr 13:5; Law 26:44-45; Yon 4:2

[n]**4:32** Kum 32:7; Mwa 1:27; Isa 45:12; Kum 28:64; 30:1; Yer 9:16; Mt 24:31; 2Sam 7:23; Ay 8:8

[o]**4:33** Kut 20:22; Kum 5:24-26

kama mlivyosikia, nao wakaishi? 34 [a]Je,
kuna mungu yeyote amepata kujaribu
mwenyewe kuchukua taifa moja kutoka
taifa lingine, kwa mapigo, kwa ishara za
miujiza na maajabu, kwa vita, kwa mkono
wenye nguvu na mkono ulionyooshwa au
kwa matendo makuu ya kutisha, kama yale
ambayo BWANA Mungu wenu aliyofanya
kwa ajili yenu huko Misri mbele ya macho
yenu?
35 [b]Mlionyeshwa mambo haya ili mpate
kujua kuwa BWANA ndiye Mungu; hakuna
mwingine ila yeye. 36 [c]Kutoka mbinguni
amewasikizisha sauti yake ili kuwaadilisha.
Hapa duniani aliwaonyesha moto wake
mkubwa, nanyi mlisikia maneno yake
kutoka kwenye ule moto. 37 [d]Kwa sababu
aliwapenda baba zenu na alichagua wazao
wao baada yao, aliwatoa katika nchi ya
Misri kwa Uwepo wake na kwa uwezo wake
mkuu, 38 [e]aliwafukuza mbele yenu mataifa
makubwa na yenye nguvu kuliko ninyi na
kuwaleta ninyi katika nchi yao na akawapa
ninyi kuwa urithi wenu, kama ilivyo leo.
39 [f]Kubalini na mweke moyoni leo kuwa
BWANA ndiye Mungu mbinguni juu na
duniani chini. Hakuna mwingine. 40 [g]Mshike
amri na maagizo yake ninayowapa leo, ili
mpate kufanikiwa ninyi na watoto wenu
baada yenu, na mpate kuishi maisha marefu
katika nchi awapayo BWANA Mungu wenu
siku zote.

*Miji Ya Makimbilio*

41 [h]Kisha Mose akatenga miji mitatu
mashariki ya Yordani, 42 [i]ambayo mtu
yeyote aliyemuua mtu angeweza kukimbilia
ikiwa amemuua jirani yake bila kukusudia
na bila kuwa na chuki naye siku zilizopita.
Angeweza kukimbilia katika mmojawapo
ya miji hii na kuokoa maisha yake. 43 [j]Miji
hiyo ilikuwa: Bezeri katika tambarare ya
jangwa kwa ajili ya Wareubeni; Ramothi
katika nchi ya Gileadi kwa ajili ya Wagadi;
nao mji wa Golani katika nchi ya Bashani
kwa ajili ya Wamanase.

*Utangulizi Wa Sheria*

44 Hii ndiyo sheria Mose aliyoweka mbele
ya Waisraeli. 45 Haya ndiyo masharti, amri
na sheria Mose aliyowapa wana wa Israeli
wakati walitoka Misri, 46 [k]nao walikuwa
katika bonde karibu na Beth-Peori mashariki
ya Yordani, katika nchi ya Sihoni mfalme
wa Waamori, ambaye alitawala Heshboni,
naye alishindwa na Mose na Waisraeli
walipokuja toka Misri. 47 [l]Waliimiliki nchi
yake na nchi ya Ogu mfalme wa Bashani,
wafalme wawili Waamori waliotawala
mashariki ya Yordani. 48 [m]Nchi hii ilienea
kutoka Aroeri ukingoni mwa Bonde la
Arnoni mpaka Mlima Sioni (yaani Hermoni),
49 pamoja na eneo lote la Araba mashariki
ya Yordani, na kuenea mpaka Bahari ya
Araba kwenye miteremko ya Pisga.

*Amri Kumi*

**(Kutoka 20:1-17)**

5 [n]Mose akawaita Israeli wote, akawaambia:
Ee Israeli, sikilizeni amri na sheria
ninazowatangazia leo. Jifunzeni, na mwe
na hakika kuzifuata. 2 [o]BWANA Mungu
wetu alifanya Agano nasi katika mlima

---

[a]**4:34** Kut 14:30; Isa 7:12; Kut 4:17; Kum 7:19; 26:8; 29:3; 1Nya 16:12; Za 9:1; 40:5; Yer 32:20; Kut 32:20; 3:20; Kum 5:15; 6:21; 15:15; Kut 15:1; Kum 34:12; Za 45:4; 65:5
[b]**4:35** Kum 4:39; 7:9; 32:4-12; Kut 8:10; 1Sam 2:2; 1Fal 8:60; 2Fal 19:19; Isa 3:10; Mk 12:32
[c]**4:36** Kut 19:19; Kum 8:5; Kut 19:20; 18:22; 24:16; 1Nya 29:1; 2Nya 20:6; Ebr 12:18, 25
[d]**4:37** Kum 7:8; 10:15; 23:5; 33:3; Za 44:3; Yer 31:3; Hos 11:1; Mal 1:2; 2:11; Kut 3:20; 13:3, 9-14
[e]**4:38** Hes 34:14-15; Kum 7:1; 9:5
[f]**4:39** Kum 8:10; Kut 15:11; Yos 2:11; Isa 42:8; Dan 4:35
[g]**4:40** Law 22:31; Mwa 26:5; Kum 5:29; 11:1; Za 105:45; Isa 48:18; Kum 5:16; 12:25; Isa 3:10; Kut 23:26; Efe 6:2-3
[h]**4:41** Hes 35:6
[i]**4:42** Kut 21:13
[j]**4:43** Yos 21:38; 1Fal 22:3; 2Fal 8:28; 9:14
[k]**4:46** Hes 21:26; Kum 3:29
[l]**4:47** Hes 21:25; Kum 3:3, 4
[m]**4:48** Kum 2:36; 3:8-9; Za 133:3
[n]**5:1** Kut 18:20
[o]**5:2** Kut 19:5

wa Horebu. 3 [a]Si kwamba BWANA alifanya
Agano na baba zetu, bali alifanya nasi, nasi
sote ambao tuko hai hapa leo. 4 [b]BWANA
alisema nanyi uso kwa uso kutoka moto juu
ya mlima. 5 [c](Wakati huo nilisimama kati
ya BWANA na ninyi kuwatangazia neno la
BWANA, kwa sababu mliogopa ule moto,
nanyi hamkupanda mlimani.) Naye Mungu
alisema:

6 [d]"Mimi ndimi BWANA Mungu
wako, niliyekutoa katika nchi ya
Misri, kutoka nchi ya utumwa.
7 [e]Usiwe na miungu mingine ila mimi.
8 [f]Usijitengenezee sanamu katika
umbo la kitu chochote kilicho
juu mbinguni au duniani chini
au ndani ya maji. 9 [g]Usivisujudie
wala kuviabudu; kwa kuwa Mimi,
BWANA Mungu wako, ni Mungu
mwenye wivu, ninayewaadhibu
watoto kwa ajili ya dhambi za
baba zao hadi kizazi cha tatu na
cha nne cha wanichukiao, 10 [h]lakini
ninaonyesha upendo kwa maelfu
ya vizazi vya wale wanipendao na
kuzishika amri zangu.
11 [i]Usilitaje bure jina la BWANA Mungu
wako, kwa kuwa BWANA hataacha
kumhesabia hatia yeye alitajaye
jina lake bure.
12 [j]Adhimisha siku ya Sabato na
kuiweka takatifu, kama BWANA
Mungu wako alivyokuagiza. 13 Kwa
siku sita utafanya kazi na kutenda
shughuli zako zote. 14 [k]Lakini siku
ya Saba ni Sabato kwa BWANA,
Mungu wako. Siku hiyo hutafanya
kazi yoyote, wewe, wala mwanao
au binti yako, wala mtumishi wa
kiume au mtumishi wa kike, wala
ng'ombe wako, punda wako au
mnyama wako yeyote, wala mgeni
aliyeko malangoni mwako, ili
kwamba mtumishi wako wa kiume
na wa kike wapate kupumzika
kama wewe. 15 [l]Kumbuka mlikuwa
watumwa huko Misri, na BWANA
Mungu wenu aliwatoa huko kwa
mkono wenye nguvu na kwa
mkono ulionyooshwa. Kwa hiyo
BWANA Mungu wako amekuagiza
kuiadhimisha siku ya Sabato.
16 [m]Waheshimu baba yako na mama
yako, kama BWANA Mungu
wako alivyokuagiza, ili siku zako
zipate kuwa nyingi na kufanikiwa
katika nchi BWANA Mungu wako
anayokupa.
17 [n]Usiue.
18 [o]Usizini.
19 [p]Usiibe.
20 [q]Usimshuhudie jirani yako uongo.
21 [r]Usitamani mke wa jirani yako.
Usitamani nyumba ya jirani yako
au shamba lake, mtumishi wake
wa kiume au wa kike, ng'ombe au

---

[a]**5:3** Kum 11:2-7; Hes 26:63-65; Ebr 8:9; Mt 13:17
[b]**5:4** Kut 19:9, 18-19; 20:22; Kum 4:33, 36; 34:10; Hes 14:4
[c]**5:5** Gal 3:19; Mwa 3:10; Ebr 12:18-21; Kut 20:18-21; 20:18-21; Hes 16:48; Za 106:23; Yer 30:21
[d]**5:6** Kut 13:3; 29:46; Law 26:1; Kum 6:4; Za 81:10
[e]**5:7** Kut 20:3
[f]**5:8** Law 26:1; Kum 4:15-16; Za 78:58; 97:7; Kut 20:4; Mdo 17:29
[g]**5:9** Hes 26:11; Kut 34:7; Hes 10:35; 14:18; Kut 34:7
[h]**5:10** Kut 34:2; Hes 14:18; Kum 7:9; Neh 1:5; Yer 32:18; Dan 9:4
[i]**5:11** Za 139:20; Law 19:12; Kum 10:20; Mt 5:33-37
[j]**5:12** Kut 16:23-30; 31:13; Mk 2:27-28; Kut 20:8
[k]**5:14** Mwa 2:2; Mt 12:2; Mk 2:17; Ebr 4:4; Ay 31:13; Yer 34:9-11; 17:21-24
[l]**5:15** Mwa 15:13; Kut 6:1; Za 108:6; Yer 32:21; Kum 4:34
[m]**5:16** Mal 1:6; Kut 21:17; Law 19:3; Eze 22:7; Mt 15:4; 19:19; Mk 7:10; 10:19; Lk 18:20; Efe 6:2-3; Kum 4:40; 11:9; Mit 3:1-2
[n]**5:17** Mwa 9:6; Law 24:17; Mhu 3:3; Yer 40:15; 41:3; Mt 5:21-22; 19:19; Mk 10:19; Lk 18:20; Rum 13:9; Yak 2:11
[o]**5:18** Law 20:10; Mt 5:27-30; 19:18; Mk 10:19; Lk 18:20; Rum 13:9; Yak 2:11
[p]**5:19** Law 19:11; Mt 19:19; Mk 10:19; Lk 18:20; Rum 13:9
[q]**5:20** Kut 23:1; Mt 19:18; Mk 10:19; Lk 18:20
[r]**5:21** Rum 7:7; 13:9

punda wake, wala kitu chochote
cha jirani yako."

22 [a]Hizi ndizo amri alizozitangaza BWANA
kwa sauti kubwa kwa kusanyiko lenu lote
huko mlimani kutoka kwenye moto, wingu
na giza nene, wala hakuongeza chochote
zaidi. Kisha akaziandika juu ya vibao viwili
vya mawe, naye akanipa mimi.

### *Woga Wa Watu Mlimani*

**(Kutoka 20:18-21)**

23 [b]Mliposikia sauti kutoka kwenye giza,
mlima ulipokuwa ukiwaka moto, viongozi
wenu wote wa makabila yenu na wazee
wenu walinijia mimi. 24 [c]Nanyi mkasema,
"BWANA Mungu wetu ametuonyesha
utukufu na enzi yake, nasi tumesikia sauti
yake kutoka kwenye moto. Leo tumeona
kwamba mwanadamu anaweza kuishi
hata kama Mungu akizungumza naye.
25 [d]Lakini sasa, kwa nini tufe? Moto huu
mkubwa utatuteketeza sisi na tutakufa
kama tukiendelea kusikia sauti ya BWANA
Mungu wetu zaidi. 26 [e]Ni mtu yupi mwenye
mwili ambaye amewahi kuisikia sauti ya
Mungu aliye hai akizungumza kutoka
kwenye moto, kama sisi tulivyoisikia,
naye akaishi? 27 [f]Sogea karibu usikie yale
yote asemayo BWANA Mungu wetu. Kisha
utuambie chochote kile ambacho BWANA
Mungu wetu anakuambia. Tutasikiliza na
kutii."

28 [g]BWANA aliwasikia wakati
mlipozungumza nami, na BWANA
akaniambia, "Nimesikia kile hawa watu
walichokuambia. Kila kitu walichokisema
ni kizuri. 29 [h]Laiti kama mioyo yao ingekuwa
na mwelekeo wa kuniogopa na kuzishika
amri zangu zote daima, ili kwamba
wafanikiwe wao pamoja na watoto wao
milele!

30 [i]"Nenda uwaambie warudi kwenye
mahema yao. 31 [j]Lakini wewe baki hapa
pamoja nami ili niweze kukupa maagizo
yote, amri na sheria ambazo utawafundisha
wazifuate katika nchi ninayokwenda
kuwapa waimiliki."

32 [k]Hivyo kuweni waangalifu kuyafanya
yale BWANA Mungu wenu aliyowaagiza;
msigeuke upande wa kuume wala wa
kushoto. 33 [l]Fuateni yale yote ambayo
BWANA Mungu wenu aliwaagiza, ili mpate
kuishi, kustawi na kuziongeza siku zenu
katika nchi mtakayoimiliki.

### *Mpende BWANA Mungu Wako*

6 Haya ndiyo maagizo, amri na sheria
ambazo BWANA Mungu wenu aliniagiza
niwafundishe ninyi ili mpate kuyashika
katika nchi ambayo ninyi mnavuka Yordani
kuimiliki, 2 [m]ili kwamba ninyi, watoto wenu
na watoto wao baada yao wamche BWANA
Mungu wenu siku zote kwa kushika amri na
maagizo yake yote ninayowapa, ili mweze
kuyafurahia maisha marefu. 3 [n]Sikia, ee
Israeli, nawe uwe mwangalifu kutii ili upate
kufanikiwa na kuongezeka sana katika nchi
itiririkayo maziwa na asali, kama BWANA,
Mungu wa baba zenu, alivyowaahidi ninyi.

4 [o]Sikia, ee Israeli: BWANA Mungu wako,
BWANA ni mmoja. 5 [p]Mpende BWANA

---

[a]**5:22** Kut 20:21; 24:12; 31:18; Kum 4:13
[b]**5:23** Kut 3:16
[c]**5:24** Kum 4:34; 8:5; 11:2; Isa 53:4; Kum 3:24; Kut 19:19
[d]**5:25** Kut 20:18-19; Kum 18:16; Ebr 12:19
[e]**5:26** Kut 33:20; Kum 4:33; Amu 6:22-23; 13:22; Isa 6:5
[f]**5:27** Kut 19:8; 24:7
[g]**5:28** Kum 18:17
[h]**5:29** Za 81:8, 13; Yos 22:5; Za 78:7; Kum 4:1-40; 12:25; 22:7; Isa 48:18; Kum 12:25; Yer 44:4; Mt 23:37; Lk 19:42; 2Kor 5:20; 6:1; 7:1; Ebr 12:25; Yn 15:14; Ufu 22:14
[i]**5:30** Mal 4:4; Gal 3:19
[j]**5:31** Kut 24:12
[k]**5:32** Kum 4:29; 10:12; 17:11, 20; 28:14; Yos 1:7; 1Fal 15:5; 2Fal 22:2; Mit 4:27; Kum 10:12; Za 119:6; Mhu 8:12; 1Tim 4:8; Efe 6:3
[l]**5:33** Isa 3:10; Yer 7:23; 38:20; Lk 1:6; Kum 4:40
[m]**6:2** Kut 20:20; 1Sam 12:24; Kum 4:9; Mwa 26:5; Kut 20:12
[n]**6:3** Mwa 15:5; Kum 5:33; 32:13-14; Kut 3:8; 13:5; 19:5
[o]**6:4** Zek 14:9; Kum 4:35-39; Neh 9:6; Za 86:10; Isa 44:6; Mk 12:29; Yn 10:30; 1Kor 8:4; Efe 4:6; Yak 2:19
[p]**6:5** Kum 11:1, 22; Mt 22:37; Mk 12:30; Lk 10:27; 1Sam 12:24; Kum 4:29; 10:12; Yos 22:5

Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote. 6 [a]Amri hizi ninazokupa leo zitakuwa katika moyo wako. 7 [b]Wafundishe watoto wako kwa bidii. Nena kuhusu amri hizi uketipo nyumbani na wakati utembeapo njiani, ulalapo na uamkapo. 8 [c]Zifunge kama alama juu ya mkono wako, na uzifunge juu ya paji la uso wako. 9 [d]Ziandike kwenye miimo ya milango ya nyumba yako na juu ya malango yako.

10 [e]Wakati BWANA Mungu wako atakapokuleta katika nchi aliyowaapia baba zako, Abrahamu, Isaki na Yakobo, kukupa wewe, nchi kubwa, ina miji inayopendeza ambayo hukuijenga, 11 [f]nyumba zilizojaa vitu vizuri vya aina nyingi ambavyo hukuvijaza, visima ambavyo hukuchimba, na mashamba ya mizabibu na mizeituni ambayo hukupanda wewe, basi, utakapokula na kushiba, 12 [g]jihadhari usije ukamwacha BWANA, aliyekutoa katika nchi ya Misri, kutoka nchi ya utumwa.

13 [h]Utamcha BWANA Mungu wako, na umtumikie yeye peke yake na kuapa kwa jina lake. 14 Usifuate miungu mingine, miungu ya mataifa yanayokuzunguka; 15 [i]kwa kuwa BWANA Mungu wako, ambaye yuko katikati yako, ni Mungu mwenye wivu na hasira yake itawaka dhidi yako, naye atakuangamiza kutoka uso wa nchi. 16 [j]Usimjaribu BWANA Mungu wako kama ulivyofanya huko Masa. 17 [k]Utayashika maagizo ya BWANA Mungu wako kwa bidii, na masharti na amri alizokupa. 18 [l]Fanya lililo haki na jema mbele za BWANA, ili upate kufanikiwa, uweze kuingia na kuimiliki nchi nzuri ambayo BWANA aliahidi kwa kiapo kwa baba zako, 19 [m]kuwafukuza kwa nguvu adui zako mbele yako kama BWANA alivyosema.

20 [n]Siku zijazo, mtoto wako atakapokuuliza, "Ni nini maana ya masharti haya, amri na sheria hizi ambazo BWANA Mungu wako alikuagiza wewe?" 21 [o]Mwambie: "Tulikuwa watumwa wa Farao huko Misri, lakini BWANA alitutoa sisi kutoka Misri kwa mkono wenye nguvu. 22 BWANA akapeleka mbele yetu ishara za miujiza na maajabu makubwa na ya kutisha mno juu ya Misri na Farao pamoja na nyumba yake yote. 23 Lakini Mungu akatutoa huko, akatuleta na kutupa nchi hii ambayo aliwaahidi baba zetu kwa kiapo. 24 [p]BWANA akatuagiza tutii amri hizi zote na kumcha BWANA Mungu wetu, ili tupate kustawi na kuendelea kuwa hai kama ilivyo leo. 25 [q]Kama tukizitii kwa bidii amri hizi zote mbele za BWANA Mungu wetu, kama alivyotuamuru sisi, hiyo itakuwa haki yetu."

*Kuyafukuza Mataifa*

**(Kutoka 34:11-16)**

7 [r]BWANA Mungu wako akuletapo katika nchi unayoingia kuimiliki, na awafukuzapo mbele yako mataifa mengi, yaani Wahiti, Wagirgashi, Waamori, Wakanaani, Waperizi, Wahivi na Wayebusi, mataifa saba makubwa tena yenye nguvu

[a]**6:6** Kum 11:18; 30:14; 32:46; Za 26:2; 37:31; 40:8; 119:11; Mit 3:3; Isa 51:7; Yer 17:1; 31:33; Eze 40:4
[b]**6:7** Kum 4:9; 11:19; Mit 22:6; Efe 6:4
[c]**6:8** Kut 13:9; Mt 23:5; Mit 3:3; 7:3; 6:21
[d]**6:9** Kum 11:20; Isa 50:8; 57:8
[e]**6:10** Mwa 11:4; Kum 12:29; 19:1; Yos 24:13
[f]**6:11** Yer 22:13; Law 26:5; Kum 8:10; 11:29; 31:20
[g]**6:12** Kum 4:9, 23; 2Fal 17:38; Za 44:17; 78:7; 103:2
[h]**6:13** Za 33:8; 34:9; Kum 13:4; 1Sam 7:3; Yer 44:10; Mt 4:10; Lk 4:4, 8; 1Sam 20:3; Kut 20:7; Mt 5:33
[i]**6:15** Kum 4:24
[j]**6:16** Kut 17:2; Mt 4:7; Lk 4:12
[k]**6:17** Law 26:3; Kum 11:22; Za 119:4-5, 56, 100, 134, 168
[l]**6:18** 2Fal 18:6; Isa 36:7; 38:3; Kum 4:40
[m]**6:19** Kut 23:27; Yos 21:44; Za 78:53; 107:2; 136:24
[n]**6:20** Kut 10:2; 13:14
[o]**6:21** Kum 4:34
[p]**6:24** Kum 10:12; 30:6; Za 86:11; Yer 32:39; Za 27:12; 41:2; Rum 10:5
[q]**6:25** Za 103:18; 119:34, 55; Kum 24:13; Rum 9:31
[r]**7:1** Law 14:34; Kum 4:38; 20:16-18; 31:3; Mwa 15:20; 10:16; 13:7; 10:17; Yos 3:10; Mdo 13:19

kuliko wewe, [2] [a]pia BWANA Mungu
wako atakapowatia mkononi mwako na
ukawashinda, basi ni lazima uwaangamize
wote kabisa. Usifanye agano nao, wala
usiwahurumie. [3] [b]Usioane nao. Usimtoe
binti yako kuolewa na mwanawe, au
kumchukua binti yake aolewe na mwanao.
[4] [c]Kwa maana watamgeuza mwanao aache
kunifuata, ili aitumikia miungu mingine,
nayo hasira ya BWANA itawaka dhidi yako,
naye atakuangamiza ghafula. [5] [d]Hili ndilo
utakalowafanyia: Vunja madhabahu yao,
vunja mawe yao ya kuabudia, katakata
nguzo zao za Ashera na kuchoma sanamu
zao kwa moto. [6] [e]Kwa kuwa wewe ni taifa
takatifu kwa BWANA Mungu wako. BWANA
Mungu wako amekuchagua wewe kutoka
mataifa yote juu ya uso wa dunia kuwa
watu wake, hazina yake ya thamani.

[7] [f]BWANA hakuweka upendo wake juu
yenu na kuwachagua kwa sababu mlikuwa
wengi mno kuliko watu wengine, kwa
maana ninyi ndio mliokuwa wachache sana
kuliko mataifa yote. [8] [g]Lakini ni kwa sababu
BWANA aliwapenda ninyi na kutunza
kiapo alichowaapia babu zenu kwamba
atawatoa ninyi kwa mkono wenye nguvu
na kuwakomboa kutoka nchi ya utumwa,
kutoka nguvu za Farao mfalme wa Misri.
[9] [h]Basi ujue kwamba BWANA Mungu wako
ndiye Mungu; ni Mungu mwaminifu,
anayetunza Agano la upendo kwa maelfu ya
vizazi vya wale wanaompenda na kuzishika
amri zake. [10] [i]Lakini

> kwa wale wanaomchukia
> atawalipiza kwenye nyuso zao
> kwa maangamizi;
> hatachelewa kuwalipiza kwenye
> nyuso zao
> wale wamchukiao.

[11] Kwa hiyo, kuweni waangalifu kufuata
maagizo, amri na sheria ninazowapa leo.

*Baraka Za Utiifu*

**(Kumbukumbu 28:1-14)**

[12] [j]Kama mkizingatia sheria hizi na
kuzifuata kwa uangalifu, basi BWANA
Mungu wenu atatunza Agano lake la
upendo nanyi, kama alivyowaapia baba
zenu. [13] [k]Atawapenda ninyi na kuwabariki
na kuongeza idadi yenu. Atabariki uzao wa
tumbo lenu, mazao ya nchi yenu, nafaka,
divai mpya na mafuta, ndama za ng'ombe wa
makundi yenu, na kondoo za makundi yenu
katika nchi ile aliyoapa kuwapa baba zenu.
[14] [l]Mtabarikiwa kuliko mataifa mengine
yote, hakuna wanaume wala wanawake
kwenu watakaookosa watoto, wala mifugo
yenu haitakuwa tasa. [15] BWANA atawakinga
na kila ugonjwa. Mungu hatatia juu yenu
ugonjwa wowote mbaya mlioufahamu huko
Misri, lakini atatia ugonjwa juu ya wale wote
wanaokuchukia. [16] [m]Ni lazima mwangamize
watu wote ambao BWANA Mungu wenu
atawatia mikononi mwenu. Msiwatazame
kwa kuwahurumia na msiitumikie miungu
yao, kwa kuwa itakuwa mtego kwenu.

[17] [n]Mnaweza kujiuliza wenyewe "Mataifa
haya ni yenye nguvu kuliko sisi. Tutawezaje

---

[a]**7:2** Kum 2:33-34; Hes 31:17; Kum 33:27; Yos 11:11; Kut 23:32; Kum 13:8; 19:13; 25:12
[b]**7:3** Kut 34:15-16; Yos 22:16; Dan 9:7; Ezr 9:2
[c]**7:4** Amu 3:6; Kum 4:26; 6:15; Isa 9:6; Mk 12:29; Yn 1:1; 10:30; 17:3; 1Kor 8:4; Efe 4:6; Flp 2:5, 6
[d]**7:5** Kut 23:24; 24:13; Kum 12:2-3; 16:21; 30:6; Mt 22:37; Mk 12:30-32
[e]**7:6** Kut 19:6; Law 27:30; Kum 26:19; Za 30:4; 37:28; 50:5; 52:9; Kum 14:2; 1Fal 3:8; Isa 41:9; Eze 20:5; Mwa 17:7; Kut 8:22; 34:9; Isa 43:1; Rum 9:4; Tit 2:14; 1Pet 2:9; Yer 2:3
[f]**7:7** Mwa 22:17; 34:30; Kum 4:37; 10:22
[g]**7:8** Kum 4:37; 1Fal 10:9; 2Nya 2:11; Za 44:3; Kut 32:13; Hes 14:8; Rum 11:28; Kut 3:20; 6:6; 13:14
[h]**7:9** Kum 4:35; Za 18:25; 33:4; 108:4; 145:13; 146:6; Isa 49:7; Yer 42:5; Hes 11:12; 1Kor 1:9; 1Fal 8:23; 2Nya 6:14; Neh 1:5; 9:32; Kut 20:6; Kum 5:10; Dan 9:4; 2Tim 2:13
[i]**7:10** Law 26:28; Hes 10:35; Neh 1:2
[j]**7:12** Law 26:3-13; Kum 28:1-14; Za 105:8-9; Mik 7:20
[k]**7:13** Za 11:5; 146:8; Mit 15:9; Isa 51:1; Yn 14:21; Mwa 17:6; Kut 1:7; Kum 1:10; 13:17; 30:5; Za 107:38; Mwa 49:25; 27:28; Hes 18:12; Kum 28:4
[l]**7:14** Kut 23:26
[m]**7:16** Yos 6:2; 10:26; Amu 3:6; Ezr 9:1; Za 106:36; Kut 10:7; Amu 8:27
[n]**7:17** Hes 33:53

kuwafukuza?” 18 [a]Lakini msiwaogope.
Kumbukeni vyema jinsi Bwana Mungu
wenu alivyofanya kwa Farao na kwa
wote huko Misri. 19 [b]Mliona kwa macho
yenu wenyewe majaribu makubwa, ishara
za miujiza na maajabu, mkono wenye
nguvu na ulionyooshwa, ambao kwa huo
Bwana Mungu wenu aliwatoa mtoke
Misri. Bwana Mungu wenu atawafanyia
hivyo watu wote ambao mnawaogopa sasa.
20 [c]Zaidi ya hayo, Bwana Mungu wenu
atatuma manyigu miongoni mwao hadi
yale mabaki watakaojificha waangamie.
21 [d]Msiingiwe na hofu kwa sababu yao,
kwa kuwa Bwana Mungu wenu, ambaye
yupo miongoni mwenu ni mkuu naye ni
Mungu wa kutisha. 22 [e]Bwana Mungu wenu
atawafukuza mataifa hayo mbele yenu
kidogo kidogo. Hamtaruhusiwa kuwaondoa
wote kwa mara moja, la sivyo wanyama
mwitu wataongezeka na kuwa karibu nanyi.
23 [f]Lakini Bwana Mungu wenu atawatia
watu hao mikononi mwenu, akiwatia katika
kuchanganyikiwa kukubwa mpaka wawe
wameangamizwa. 24 [g]Atawatia wafalme
wao mikononi mwenu, nanyi mtayafuta
majina yao chini ya mbingu. Hakuna hata
mmoja atakayeweza kusimama dhidi yenu
bali mtawaangamiza. 25 [h]Vinyago vya
miungu yao mtavichoma moto. Msitamani
fedha wala dhahabu iliyo juu yao, wala
msizichukue kwa ajili yenu, la sivyo
mtakuwa mmetekwa navyo. Kwa kuwa
ni chukizo kwa Bwana Mungu wenu.
26 [i]Msilete vitu vya machukizo katika
nyumba zenu kwani ninyi, mtatengwa kama
vitu hivyo kwa maangamizo. Ukichukie
kabisa kitu hicho kwa kuwa kimetengwa
kwa maangamizo.

*Usimsahau Bwana*

8 [j]Uwe mwangalifu kufuata kila agizo
ninalokupa wewe leo, ili mweze kuishi,
kuongezeka na mweze kuingia mkamiliki
nchi ambayo Bwana aliahidi kwa kiapo
kwa baba zenu. 2 [k]Kumbuka jinsi Bwana
Mungu wenu alivyowaongoza katika
njia yote katika jangwa kwa miaka hii
arobaini, kukunyenyekeza na kukujaribu
ili ajue lililoko moyoni mwako, kwamba
utayashika maagizo yake au la. 3 [l]Alikudhili
na kukufanya uone njaa kisha akulishe
kwa mana, ambayo wewe wala baba zako
hamkuijua, awafundishe kuwa mwanadamu
hataishi kwa mkate tu bali kwa kila neno
litokalo katika kinywa cha Bwana.
4 [m]Nguo zenu hazikuchakaa wala miguu
yenu haikuvimba kwa miaka hii arobaini.
5 [n]Mjue basi ndani ya mioyo yenu kama
mtu anavyomwadibisha mwanawe, ndivyo
Bwana Mungu wako atawaadibisha ninyi.
6 [o]Shikeni maagizo ya Bwana Mungu
wenu mtembee katika njia zake na
kumheshimu. 7 [p]Kwa kuwa Bwana Mungu
wenu anawaleta katika nchi nzuri, nchi
yenye vijito na mabwawa ya maji, yenye
chemchemi zinazotiririka mabondeni
na katika vilima; 8 [q]nchi yenye ngano na

[a]**7:18** Hes 14:9; Kum 1:21; 29; Za 105:5; 119:52
[b]**7:19** Za 136:12; Kum 4:34
[c]**7:20** Kut 23:28; Yos 24:12
[d]**7:21** Mwa 17:7; Yos 3:10; Kum 10:17; Neh 1:5; 9:32; Za 47:2; 66:3; 68:35; Isa 9:6; Dan 9:4
[e]**7:22** Kut 23:30
[f]**7:23** Kut 23:27; Yos 10:11
[g]**7:24** Yos 10:24; 1:5; 10:8; 23:9; 21:44; Za 110:5; Kut 23:31; Kum 11:25; Ay 35:7, 8; Yer 32:39; Za 41:2; Lk 10:23
[h]**7:25** Kut 4:14; 32:20; 20:17; Yos 7:21; Amu 8:27; 1Nya 14:12; Kum 17:1; Rum 10:3
[i]**7:26** Law 27:28-29
[j]**8:1** Kum 4:1; Kut 19:5; Ay 36:11; Za 16; 11; Eze 20:19
[k]**8:2** Kum 29:5; Za 136:16; Amo 2:10; Mwa 22:1; Yos 6:17; 11:11; Kut 23:32; Amu 1:24; 2:2
[l]**8:3** Isa 2:11; Yer 44:10; Kut 16:14; 1Fal 8:36; Za 25:5; 94:12; 119:171; Mwa 3:19; Ay 23:12; Za 104:15; Mit 28:21; Isa 51:14; Yer 42:14; Ay 22:22; Za 119:13; 138:4; Kut 16:2-3; Mt 4:4; Lk 4:4
[m]**8:4** Kum 29:5; Neh 9:21
[n]**8:5** Kum 4:36; 2Sam 7:14; Ay 5:17; 33:19; Mit 3:11-12; Ebr 12:5-11; Ufu 3:19
[o]**8:6** Kut 33:13; 1Fal 3:14; Za 81:13; 95:10; Kum 5:33
[p]**8:7** Za 106:24; Yer 3:19; Eze 20:6; Kum 11:9-12; Yer 2:7
[q]**8:8** Kut 9:31; Mwa 49:11; Hes 13:23; 1Fal 4:25; Kum 32:13; Za 81:16

shayiri, mizabibu na mitini, mikomamanga,
mafuta ya zeituni na asali; 9 [a]nchi ambayo
chakula hakitapungua na hamtakosa
chochote; nchi ambayo miamba yake ni
chuma na mnaweza kuchimba shaba kutoka
kwenye vilima.

10 [b]Wakati mtakapokwisha kula na
kushiba, msifuni BWANA Mungu wenu
kwa ajili ya nchi nzuri aliyowapa.
11 [c]Jihadharini msimsahau BWANA Mungu
wenu, mkashindwa kushika maagizo yake,
sheria na amri zake ambazo ninawapa
leo. 12 [d]Angalia wakati mtakapokuwa
mmekula na kushiba, mkajenga nyumba
nzuri na kukaa humo, 13 na wakati makundi
yenu ya ng'ombe na mbuzi na kondoo
yatakapoongezeka na fedha na dhahabu
yenu itakapoongezeka na vyote mlivyo
navyo vitakapozidishwa, 14 [e]basi mioyo yenu
isiwe na kiburi mkamsahau BWANA Mungu
wenu aliyewatoa katika nchi ya Misri,
kutoka nchi ya utumwa. 15 [f]Aliwaongoza
kupitia jangwa lile kubwa na la kutisha,
nchi ile ya kiu isiyo na maji, yenye nyoka
wa sumu na nge. Aliwatolea maji kutoka
kwenye mwamba mgumu. 16 [g]Aliwapa
mana ya kula jangwani, kitu ambacho baba
zenu hawakukijua, ili kuwanyenyekesha
na kuwajaribu ninyi ili mwishoni apate
kuwatendea mema. 17 [h]Mnaweza kusema,
"Uwezo wangu na nguvu za mikono yangu
ndizo zilizonipatia utajiri huu." 18 [i]Lakini
kumbukeni BWANA Mungu wenu, ndiye
ambaye huwapa uwezo wa kupata utajiri,
na hivyo kulithibitisha Agano lake, ambalo
aliwaapia baba zenu, kama ilivyo leo.

19 [j]Ikiwa mtamsahau BWANA Mungu wenu,
mkaifuata miungu mingine, mkaiabudu na
kuisujudia, ninashuhudia dhidi yenu leo
kwamba hakika mtaangamizwa. 20 [k]Kama
mataifa BWANA aliyoyaangamiza mbele
yenu, ndivyo ninyi mtakavyoangamizwa
kwa kutokumtii BWANA Mungu wenu.

*Si Kwa Sababu Ya Haki Ya Waisraeli*

**(Kutoka 32:1-35)**

9 [l]Sikiliza, ee Israeli. Sasa mnakaribia
kuvuka Yordani mwingie na kuwafukuza
mataifa makubwa na yenye nguvu kuliko
ninyi pamoja na miji mikubwa yenye kuta
zilizofika juu angani. 2 [m]Watu ni wenye
nguvu na warefu, ni wana wa Waanaki!
Mnafahamu habari zao na mmesikia
inavyosemekana: "Ni nani awezaye
kusimama dhidi ya Waanaki?" 3 [n]Kuweni
na hakika leo kwamba BWANA Mungu
wenu ndiye atakayetangulia kuvuka
mbele yenu kama moto uteketezao.
Atawaangamiza; atawatiisha mbele yenu.
Nanyi mtawafukuza na kuwaangamiza
mara moja, kama BWANA alivyowaahidi.

4 [o]Baada ya BWANA Mungu wenu
kuwafukuza mbele yenu, msiseme mioyoni
mwenu, "BWANA ametuleta hapa kuimiliki
nchi hii kwa sababu ya haki yetu." La, ni
kwa sababu ya uovu wa mataifa haya ndiyo
BWANA anawafukuza mbele yenu. 5 [p]Si kwa
sababu ya haki yenu wala uadilifu wenu
kwamba mtaimiliki nchi yao; lakini kwa

---

[a]**8:9** Amu 18:10; Ay 28:2
[b]**8:10** Kum 6:10-12
[c]**8:11** Kum 4:9
[d]**8:12** Mit 30:9; Hos 13:6
[e]**8:14** Za 78:7; 106:21
[f]**8:15** Kum 1:19; 32:13; 32:10; Hes 21:6; Isa 14:29; 30:6; Kut 17:6; Ay 28:9; Za 78:15; 114:8
[g]**8:16** Kut 16:14; 16:15; Mwa 22:1; Rum 8:28; 2Kor 4:17; Ebr 12:11; Yak 1:12; 1Pet 1:7
[h]**8:17** Kum 9:4, 24; 31:27; Amu 7:2; Za 44:3; Isa 10:13
[i]**8:18** Mwa 26:13; Kum 26:10; 28:4; 1Sam 2:7; Za 25:13; 112:3; Mit 8:18; 10:22; Mhu 9:11; Hos 2:8
[j]**8:19** Kum 6:14; 4:26; 30:18; Za 16:4; Yer 7:6; 13:10; 25:6
[k]**8:20** 2Fal 21:2; Za 10:16; Eze 5:5-17; Mao 1:1-22; 2:17; Dan 9:12; Zek 1:6
[l]**9:1** Hes 35:10; Kum 1:28; 4:38; 11:23, 31; Hes 13:28; Mwa 11:4
[m]**9:2** Hes 13:22; Yos 11:12
[n]**9:3** Kum 7:23-24; 31:3; Yos 3:11; Kut 15:7; 19:18; 23:31; Ebr 12:29; Mik 2:13; Ufu 19:11-15; Isa 30:27; 33:14; Nah 1:5, 6; 2The 1:8; Kut 23:31
[o]**9:4** Kum 8:17; 18:9-14; 2Fal 16:3; 17:8; 21:2; Ezr 9:11; Kut 23:24; Law 18:21-24, 30; Eze 36:32; Rum 11:6; 1Kor 4:4; Mwa 15:16
[p]**9:5** Efe 2:9; Kum 18:9; 4:38; 11:22; Law 18:25; Mwa 12:7; 13:15; 26:4; Eze 36:32; Tit 3:5; 2Tim 1:9; Lk 1:54; Mdo 13:32, 33; Rum 15:8

sababu ya uovu wa mataifa haya, BWANA
Mungu wenu atawafukuza mbele yenu,
ili kutimiza lile alilowaapia baba zenu
Abrahamu, Isaki na Yakobo. [6] [a]Basi mjue,
si kwa sababu ya haki yenu BWANA Mungu
wenu anawapa nchi hii nzuri kuimiliki, kwa
kuwa ninyi ni taifa lenye shingo ngumu.

*Ndama Ya Dhahabu*

[7] [b]Kumbukeni hili, kamwe msisahau jinsi
mlivyomkasirisha BWANA Mungu wenu
kwa hasira huko jangwani. Tangu siku
mlipotoka Misri mpaka mlipofika hapa,
mmekuwa waasi dhidi ya BWANA. [8] [c]Kule
Horebu mliamsha ghadhabu ya BWANA,
kwa hiyo alikasirika vya kutosha hata
akataka kuwaangamiza. [9] [d]Nilipopanda
mlimani kupokea mbao za mawe, mbao
za Agano lile BWANA alilofanya nanyi,
nilikaa mlimani siku arobaini usiku na
mchana, sikula mkate wala sikunywa maji.
[10] [e]BWANA alinipa mbao mbili za mawe
zilizoandikwa kwa kidole cha Mungu. Juu
ya mbao hizo kulikuwepo amri zote ambazo
BWANA aliwatangazia kule mlimani kwa
njia ya moto, siku ya kusanyiko.
[11] [f]Mwisho wa siku arobaini usiku na
mchana, BWANA alinipa mbao mbili za
mawe, mbao za Agano. [12] [g]Kisha BWANA
akaniambia, "Shuka chini mara moja, kwa
sababu watu wako ambao umewatoa katika
nchi ya Misri wamepotoka. Wamegeukia
mbali haraka kutoka lile nililowaagiza,
wamejitengenezea sanamu ya kusubu."
[13] [h]Naye BWANA akaniambia,
"Nimewaona watu hawa nao ni watu wenye
shingo ngumu sana! [14] [i]Niache, ili nipate
kuwaangamiza na kufuta jina lao kutoka
chini ya mbingu. Nami nitakufanya kuwa
taifa lenye nguvu zaidi na kuwa wengi
kuliko wao."
[15] [j]Kwa hiyo niligeuka na kuteremka
kutoka mlimani kwani mlima ulikuwa
ukiwaka moto. Pia vibao vile viwili vya
Agano vilikuwa mikononi mwangu.
[16] [k]Nilipotazama, niliona kuwa mmefanya
dhambi dhidi ya BWANA Mungu wenu;
mmejifanyia sanamu ya kusubu katika
umbo la ndama. Mmegeuka upesi kutoka
njia ile BWANA aliyowaagiza. [17] [l]Kwa hiyo
nilichukua vibao vile viwili nikavitupa na
kuvipasua vipande vipande mbele ya macho
yenu.
[18] [m]Ndipo tena nikasujudu mbele za
BWANA kwa siku arobaini usiku na
mchana. Sikula mkate wala sikunywa maji,
kwa sababu ya dhambi yote mliyoifanya,
mkifanya lile lililo ovu mbele za BWANA
na kumkasirisha. [19] [n]Niliogopa hasira
na ghadhabu ya BWANA, kwa kuwa
aliwakasirikia vya kutosha na kutaka
kuwaangamiza. Lakini BWANA alinisikiliza
tena. [20] Bali yeye alimkasirikia Aroni
kiasi cha kutaka kumwangamiza, nami
wakati huo nilimwombea Aroni pia.
[21] [o]Kisha nikachukua ile sanamu ya ndama
mliyoitengeneza na kuichoma kwenye
moto. Nikaiponda na kuisaga ikawa unga
laini kama vumbi, nikatupa lile vumbi
kwenye kijito kilichotiririka toka mlimani.
[22] [p]Pia mlimkasirisha BWANA huko
Tabera, Masa na Kibroth-Hataava.
[23] [q]Vilevile wakati BWANA alipowatuma
kutoka Kadesh-Barnea, alisema, "Kweeni,
mkaimiliki nchi ambayo nimewapa." Lakini
mliasi dhidi ya agizo la BWANA Mungu
wenu. Hamkumtegemea wala kumtii.

[a]**9:6** Kut 32:9; Mdo 7:51
[b]**9:7** Hes 11:33; Kut 23:21; 14:11
[c]**9:8** Hes 16:46; 1Sam 28:18; Ay 20:28; Za 2:12; 7:11; 69:24; 110:5; 106:19; Isa 9:19; Eze 20:13; Kut 32:12; Ezr 9:14
[d]**9:9** Kum 9:13; Mwa 7:4; Kut 24:12-18; 34:28; Lk 4:1
[e]**9:10** Kut 31:18; Kum 10:4; 18:16
[f]**9:11** Mwa 7:4; Kut 24:12
[g]**9:12** Kum 4:16; Amu 2:17; Kut 32:7-8
[h]**9:13** Kut 32:9; Kum 10:16; 2Fal 17:14
[i]**9:14** Kut 34:10; Hes 14:12; Yer 7:16; Kum 29:20; Za 9:5; 109:13
[j]**9:15** Kut 19:18; 32:15
[k]**9:16** Kut 32:4, 9
[l]**9:17** Za 69:9; 119:139
[m]**9:18** Kut 34:28; 32:31
[n]**9:19** Kut 32:14; Ebr 12:21; Kut 34:10; Hes 11:2; 1Sam 7:9; Yer 15:1; Kum 9:26; 10:10; Za 106:23; Yak 5:15; Amo 7:1-6
[o]**9:21** Za 18:42; Isa 2:18; 29:5; 40:15; Kut 32:20; Mk 1:7; Hos 8:11
[p]**9:22** Hes 1:53; 11:3; 11:34; Kut 17:7
[q]**9:23** Kum 1:32; Hes 14:9; Za 106:24; Hes 13:3; 14:1; Za 78:22; Ebr 3:18, 19; 4:2

24 [a]Mmekuwa waasi dhidi ya BWANA tangu
nilipowajua ninyi.
25 [b]Nilianguka kifudifudi mbele za BWANA
kwa zile siku arobaini usiku na mchana
kwa sababu BWANA alikuwa amesema
angewaangamiza ninyi. 26 [c]Nilimwomba
BWANA na kusema, “Ee BWANA Mwenyezi,
usiangamize watu wako, urithi wako
mwenyewe ule ulioukomboa kwa uweza
wako mkuu na kuwatoa katika nchi ya Misri
kwa mkono wenye nguvu. 27 [d]Wakumbuke
watumishi wako Abrahamu, Isaki na
Yakobo. Usiangalie ukaidi wa watu hawa,
uovu wao wala dhambi yao. 28 [e]Watu wa
nchi ile uliyotutoa sisi wasije wakasema, ‘Ni
kwa sababu BWANA hakuweza kuwachukua
mpaka nchi aliyokuwa amewaahidia, kwa
sababu aliwachukia, akawaleta ili aje
kuwaua jangwani.’ 29 [f]Bali wao ni watu
wako, urithi wako ule ulioutoa Misri kwa
uweza wako mkuu na kwa mkono wako
ulionyooka.”

*Vibao Vingine Vya Amri Kumi*

**(Kutoka 34:1-10)**

10 [g]Wakati ule BWANA aliniambia,
“Chonga vibao viwili vya mawe
kama vile vya kwanza uje kwangu juu
mlimani. Pia utengeneze Sanduku la
mbao. 2 [h]Nitaandika juu ya vibao maneno
yaliyokuwa katika vile vibao vya kwanza,
ambavyo ulivivunja. Kisha utaviweka ndani
ya Sanduku.”
3 [i]Hivyo nikatengeneza Sanduku kwa mti
wa mshita, nikachonga pia vibao vya mawe
kama vile vya kwanza, kisha nikakwea
mlimani nikiwa na vibao viwili mikononi
mwangu. 4 [j]BWANA akaandika juu ya hivi
vibao kile alichokuwa amekiandika kabla,
Amri Kumi alizokuwa amewatangazia
juu mlimani, kutoka kwenye moto siku
ile ya kusanyiko. BWANA akanikabidhi.
5 [k]Kisha nikashuka kutoka mlimani
na kuweka vibao ndani ya Sanduku
nililokuwa nimelitengeneza, kama BWANA
alivyoniagiza, navyo viko huko sasa.
6 [l](Waisraeli walisafiri kutoka visima vya
Yaakani hadi Mosera. Huko Aroni alifariki
na kuzikwa, naye Eleazari mwanawe
akachukua nafasi yake kama kuhani.
7 [m]Kutoka pale, walisafiri hadi Gudgoda
wakaendelea mpaka Yotbatha, nchi yenye
vijito vya maji. 8 [n]Wakati huo BWANA
aliteua kabila la Lawi kulibeba Sanduku
la Agano la BWANA, kusimama mbele za
BWANA ili kutoa huduma, na kutangaza
baraka kwa Jina lake, kama wanavyofanya
mpaka leo. 9 [o]Hiyo ndiyo sababu ya Walawi
kutokuwa na sehemu wala urithi miongoni
mwa ndugu zao; BWANA ndiye urithi wao,
kama BWANA Mungu wao alivyowaambia.)
10 [p]Basi nilikaa mlimani kwa siku arobaini
usiku na mchana, kama nilivyofanya
mara ya kwanza, pia BWANA alinisikiliza
hata wakati huu. Haikuwa nia yake
kuwaangamiza. 11 BWANA akaniambia,
“Nenda, ukawaongoze watu katika njia yao
ili kwamba waweze kuingia na kuimiliki
nchi ile niliyowaapia baba zao kuwapa.”

*Mche BWANA*

12 [q]Na sasa, ee Israeli, BWANA Mungu

[a]**9:24** Kum 8:17; 31:27
[b]**9:25** Mwa 7:4; Kut 33:17
[c]**9:26** Kut 33:13; 34:9; 6:6; 32:11; Kum 15:15; 2Sam 7:23; Za 78:35; 1Sam 7:9; Mit 15:29; Yer 15:1
[d]**9:27** Kut 32:9
[e]**9:28** Kum 32:27; 1:27; Kut 32:12; Yos 7:9; Hes 14:16; Mwa 41:57; 1Sam 14:25; Yos 7:7-9; Za 115:1, 2; Isa 48:9-11
[f]**9:29** Kut 33:13; 34:9; Kum 32:9; 4:34; Neh 1:10; Yer 27:5; 32:17; 1Fal 8:51; Neh 1:10; Za 95:7
[g]**10:1** Kut 34:2; 25:10
[h]**10:2** Kut 25:16, 21; 2Nya 5:10; 6:11
[i]**10:3** Kut 37:1-9; 34:4; 26:5
[j]**10:4** Kut 24:12; 34:28; 20; 1; Kum 9:10; Yer 31:33
[k]**10:5** Kut 19:11; 25:10; 25:21; 34:29; 40:21; 1Sam 8:3; 1Fal 8:9
[l]**10:6** Hes 33:30; 27:13; 20:25-28; Kut 6:23
[m]**10:7** Hes 33:32-34; Za 42:1; Wim 5:12; Isa 32:2
[n]**10:8** Hes 3:6; 10:33; 16:9; Mwa 48:20; 1Nya 23:26; Kum 18:5; 21:5; Law 9:22
[o]**10:9** Hes 18:20; Eze 44:28
[p]**10:10** Kut 33:17; 34:28; Kum 9:18-19; 25
[q]**10:12** Mik 6:8; Kut 20:20; 1Fal 2:3; 3:3; 4:4; Kum 5:32; 5:33; 6:13; 6:5; 11:13; 28:47; Mt 22:37; 1Tim 1:5; Za 100:2; Kum 6:5; Za 119:2; Kum 5:32

wako anataka nini kwako ila kumcha
Bwana Mungu wako, kwenda katika njia
zake, kumpenda na kumtumikia Bwana
Mungu wako kwa moyo wako wote na kwa
roho yako yote, 13 [a]na kuyashika maagizo ya
Bwana na amri zake ninazokupa leo kwa
mafanikio yako mwenyewe?
14 [b]Mbingu, hata mbingu za juu sana,
dunia na kila kitu kilichomo ndani yake,
ni mali ya Bwana Mungu wako. 15 [c]Hata
hivyo Bwana alikuwa na shauku na
baba zako, akawapenda na akawachagua
ninyi, wazao wao, kuliko mataifa yote,
kama ilivyo leo. 16 [d]Kwa hiyo tahirini
mioyo yenu, na msiwe na shingo ngumu
tena. 17 [e]Kwa kuwa Bwana Mungu wenu
ni Mungu wa miungu na Bwana wa
mabwana, Mungu mkuu, mwenye uweza
na wa kutisha, ambaye hana upendeleo na
hapokei rushwa. 18 [f]Huwapigania yatima na
wajane, humpenda mgeni, akimpa chakula
na mavazi. 19 [g]Nanyi wapendeni wageni,
kwa kuwa ninyi wenyewe mlikuwa wageni
huko Misri. 20 [h]Mche Bwana Mungu wako
na umtumikie yeye. Shikamana naye kwa
uthabiti na kuapa kwa jina lake. 21 [i]Yeye
ni sifa yako; yeye ni Mungu wako, ambaye
alikutendea yale maajabu makubwa na
ya kutisha uliyoyaona kwa macho yako
mwenyewe. 22 [j]Baba zako walioshuka
kwenda Misri jumla yao walikuwa sabini,
na sasa Bwana Mungu wako amekufanya
wengi kama nyota za angani.

*Mpende Na Umtii Bwana*

11 [k]Mpende Bwana Mungu wako na
kushika masharti yake, amri zake,
sheria zake na maagizo yake siku zote.
2 [l]Kumbuka hivi leo kwamba sio watoto
wako walioona na kujua adhabu ya Bwana
Mungu wako: utukufu wake, mkono wake
wenye nguvu, mkono wake ulionyooshwa;
3 ishara alizozifanya na mambo aliyoyafanya
katikati ya Misri, kwa Farao mfalme wa Misri
na kwa nchi yake yote; 4 [m]lile alilolifanyia
jeshi la Wamisri, farasi na magari yake,
jinsi alivyowafurikisha na maji ya Bahari ya
Shamu walipokuwa wakiwafuatilia ninyi,
na jinsi Bwana alivyowaletea angamizo
la kudumu juu yao. 5 Sio watoto wenu
walioyaona yale Mungu aliyowafanyia
huko jangwani mpaka mkafika mahali hapa,
6 [n]wala lile Mungu alilowafanyia Dathani
na Abiramu, wana wa Eliabu wa kabila la
Reubeni, wakati ardhi ilipofungua kinywa
chake katikati ya Israeli yote, ikawameza
pamoja na walio nyumbani mwao, hema
zao na kila kitu kilichokuwa hai ambacho
kilikuwa mali yao. 7 [o]Bali ilikuwa ni macho
yenu wenyewe ambayo yaliyaona mambo
haya yote makuu Bwana aliyoyatenda.
8 [p]Kwa hiyo fuateni maagizo yote
ninayowapa leo, ili mpate kuwa na nguvu
za kuingia na kuiteka nchi ile ambayo
mnavuka Yordani kuimiliki, 9 [q]ili mpate
kuishi siku nyingi katika nchi ile ambayo
Bwana aliapa kuwapa baba zenu na wazao
wao, nchi itiririkayo maziwa na asali.

[a]**10:13** Kum 4:2; 5:33; 6:25
[b]**10:14** Za 148:4; Isa 19:1; Hab 3:8; Neh 9:6; Ay 35:5; Za 8:3; 89:11; 104:3; Kum 33:26; Za 115:16; 1Fal 8:27; Kut 19:5; Za 24:1; Mdo 17:24
[c]**10:15** Kum 4:37; Za 105:6; 135:4; Hes 14:8; Rum 11:28; 1Pet 2:9
[d]**10:16** Mwa 17:11; Law 26:41; Kum 30:6; Yer 32:39; Kut 32:9; 9:13; Yer 4:4; Kum 9:6
[e]**10:17** Yos 22:22; Za 135:9; 136:2; Dan 2:47; 11:36; Za 136:3; 1Tim 6:15; Kum 7:21; 1:17; Mal 2:9; Kut 23:8; Law 19:16; Efe 6:9
[f]**10:18** Kut 22:21, 22-24; 23:9; Law 19:33; Kum 27:19; Ay 29:13; Za 94:6; Isa 10:2; Yer 49:11; Hes 10:32
[g]**10:19** Kum 7:12; Kut 22:21; Kum 24:19; Law 19:34; Eze 47:22-23
[h]**10:20** Mt 4:10; Kum 11:22; 13:4; 30:20; Yos 23:8; Rut 1:14; 2Fal 18:6; Za 119:31; Isa 38:3; Kut 20:7; Za 63:11
[i]**10:21** Kut 15:2; 1Sam 12:24; Za 126:2; 2Sam 7:23; Yer 17:14; Za 106:21-22
[j]**10:22** Mwa 34:30; 46:26; Mdo 7:14; Mwa 12:2; Hes 10:36
[k]**11:1** Kum 6:5; Law 8:35; Zek 3:7
[l]**11:2** Kum 31:13; Za 78:6; 136:12; Kum 3:24; 5:24; 8:5; Za 11:3; Kut 7:8-21
[m]**11:4** Kut 15:1; 14:27; Hes 21:4
[n]**11:6** Hes 16:1-35; Za 106:16-18; Isa 24:19
[o]**11:7** Kum 5:3
[p]**11:8** Ezr 9:10; Kum 31:6-7, 23; Yos 1:7
[q]**11:9** Kum 5:16; 9:5; Kut 3:8; Mit 10:27; Kum 4:40; Mit 3:1, 26

10 [a]Nchi mnayoiingia kuimiliki haifanani na
nchi ya Misri mlikotoka ambako mlipanda
mbegu yenu na kuinywesha, kama bustani
ya mboga. 11 [b]Lakini nchi mnayovuka
Yordani kuimiliki ni nchi ya milima na
mabonde inywayo mvua kutoka mbinguni.
12 [c]Ni nchi ambayo BWANA Mungu wenu
anaitunza; macho ya BWANA Mungu wenu
yanaitazama daima kutoka mwanzo wa
mwaka hadi mwisho wa mwaka.
13 [d]Hivyo kama mkiyatii maagizo yangu
ninayowapa leo kwa uaminifu, yaani
kwa kumpenda BWANA Mungu wenu, na
kumtumikia kwa moyo wako wote na kwa
roho yenu yote, 14 [e]ndipo atawanyweshea
mvua katika nchi yenu kwa majira yake,
mvua ya masika na ya vuli, ili mpate
kuvuna nafaka zenu, divai mpya na mafuta.
15 [f]Nitawapa majani kwa ajili ya ng'ombe
wenu, nanyi mtakula na kushiba.
16 [g]Jihadharini, la sivyo mtashawishika
kugeuka na kuabudu miungu mingine na
kuisujudia. 17 [h]Ndipo hasira ya BWANA
itawaka dhidi yenu, naye atafunga mbingu
ili mvua isinyeshe nayo ardhi haitatoa
mazao, nanyi mtaangamia mara katika
nchi nzuri ambayo BWANA anawapa.
18 [i]Yawekeni haya maneno yangu katika
mioyo yenu na akili zenu, yafungeni kama
alama juu ya mikono yenu na kwenye paji
za nyuso zenu. 19 [j]Wafundisheni watoto
wenu, yazungumzeni wakati mketipo
nyumbani na wakati mtembeapo njiani,
wakati mlalapo na wakati mwamkapo.
20 [k]Yaandikeni juu ya miimo ya nyumba
zenu na juu ya malango yenu, 21 [l]ili kwamba
siku zenu na siku za watoto wenu zipate
kuwa nyingi katika nchi ile BWANA aliyoapa
kuwapa baba zenu, kama zilivyo nyingi siku
za mbingu juu ya nchi.
22 [m]Kama mkishika kwa makini maagizo
haya yote ninayowapa kuyafuata, ya
kumpenda BWANA Mungu wenu, kuenenda
katika njia zake zote na kushikamana naye
kwa uthabiti, 23 [n]ndipo BWANA atawafukuza
mataifa haya yote mbele yako, nawe
utawafukuza mataifa yaliyo makubwa
na yenye nguvu kukuliko wewe. 24 [o]Kila
mahali mtakapoweka mguu wenu patakuwa
penu: Nchi yenu itaenea kutoka jangwa la
Lebanoni, na kutoka mto wa Frati hadi
bahari ya magharibi[p] 25 [q]Hapatakuwa na
mtu atakayeweza kusimama dhidi yenu.
BWANA Mungu wenu, kama alivyoahidi,
ataweka juu ya nchi yote utisho na hofu
kwa ajili yenu popote mwendako.
26 [r]Tazama, leo ninaweka mbele yenu
baraka na laana: 27 [s]baraka kama mtatii
maagizo ya BWANA Mungu wenu, ambayo
ninawapa leo; 28 [t]laana kama hamtatii
maagizo ya BWANA Mungu wenu na
kuacha njia ambayo ninawaamuru leo
kwa kufuata miungu mingine, ambayo
hamkuijua. 29 [u]Wakati BWANA Mungu
wenu atakapokuwa amewaleta katika
nchi mnayoiingia kuimiliki, mtatangaza
baraka kutoka Mlima Gerizimu, na
kutangaza laana kutoka Mlima Ebali.

[a]**11:10** Isa 11:15; 37:25; Zek 8:7
[b]**11:11** Eze 36:4; Kum 8:7; Neh 9:25
[c]**11:12** 1Fal 8:29; 9:3
[d]**11:13** Kum 6:17; 10:12; 4:29; Yer 17:24; 2The 3:5
[e]**11:14** Law 26:4; Mdo 14:17; Za 147:8; Yer 3:3; Yoe 2:23; Yak 5:7; Yer 5:24
[f]**11:15** Za 104:14; Law 26:5; Kum 6:11; Za 104:14; Yoe 2:19
[g]**11:16** Kum 4:19; 8:19; 29:18; Ay 31:9; 27
[h]**11:17** Kum 6:15; 9:19; 1Fal 17:1; 2Nya 6:26; 7:13; Law 26:20; Kum 4:26; 28:12, 24
[i]**11:18** Kut 13:9; Kum 6:6-8
[j]**11:19** Kut 12:26; Kum 6:7; Za 145:4; Isa 38:19; Yer 32:39; Kum 4:9-10
[k]**11:20** Kum 6:9; Hab 2:2
[l]**11:21** Ay 5:26; Mit 3:2; 4:10; 9:11; Za 72:5
[m]**11:22** Kum 6:17; 6:5; 10:20
[n]**11:23** Kum 9:5; 4:38; Kut 23:28; Kum 9:1
[o]**11:24** Mwa 15:18; Kum 1:36; 12:20; 19:8; Yos 1:3; 14:9; Mwa 2:14
[p]24 Yaani Bahari ya Mediterania.
[q]**11:25** Kum 2:25; Kut 23:27; Kum 7:24
[r]**11:26** Za 24:5; Law 26:14-17; Kum 27:13-26; 30:1, 15, 19; Mao 2:17; Dan 9:11; Mal 3:9; 4:6
[s]**11:27** Kum 28:1-14; Za 24:5
[t]**11:28** 2Nya 24:20; Yer 42:13; 44:16; Kum 4:28; 13:6-13; 29:26; 1Sam 26:19
[u]**11:29** Mwa 9:7; Kum 27:4; Yos 8:30; Kum 27:12-13; Yos 8:33; Yn 4:20

30 [a]Kama mnavyofahamu, milima hii
ipo ng'ambo ya Yordani, magharibi ya
barabara, kuelekea machweo ya jua, karibu
na miti mikubwa ya More, katika nchi ya
wale Wakanaani wanaoishi Araba, jirani
na Gilgali. 31 [b]Karibu mvuke ng'ambo ya
Yordani kuingia na kuimiliki nchi ambayo
BWANA Mungu wenu anawapa. Wakati
mtakapokuwa mmeichukua na mnaishi
humo, 32 hakikisheni kwamba mnatii amri
na sheria zote ninazoziweka mbele yenu
leo.

*Mahali Pekee Pa Kuabudia*

12 [c]Hizi ndizo amri na sheria ambazo
ni lazima mwe waangalifu kuzifuata
katika nchi ambayo BWANA, Mungu wa baba
zenu, amewapa kumiliki, kwa muda wote
mtakaoishi katika nchi. 2 [d]Haribuni kabisa
kila mahali pao pa kuabudia kwenye milima
mirefu, vilima na chini ya kila mti mkubwa
ambamo mataifa haya mnayokwenda
kuchukua ardhi yao huabudia miungu yao.
3 [e]Bomoeni madhabahu zao, vunjeni yale
mawe wanayoabudu, chomeni moto nguzo
zao za Ashera; katilieni mbali sanamu za
miungu yao na mfute majina yao mahali
hapo.
4 [f]Kamwe msimwabudu BWANA Mungu
wenu kama wanavyoabudu wao. 5 [g]Bali
mtatafuta mahali BWANA Mungu wenu
atakapopachagua katika makabila yenu
yote ili aliweke jina lake huko kuwa
makao yake. Mahali hapo ndipo iwapasapo
kwenda; 6 [h]hapo ndipo mtakapoleta sadaka
zenu za kuteketezwa na dhabihu, zaka zenu
na changizo zenu, kile ulichoweka nadhiri
kutoa, sadaka zenu za hiari na malimbuko
ya makundi yenu ya ng'ombe pamoja na
mbuzi na kondoo. 7 [i]Hapo, katika uwepo
wa BWANA Mungu wenu, ninyi pamoja na
jamaa zenu, mtakula na kufurahia kila kitu
ambacho mmegusa kwa mikono yenu, kwa
sababu BWANA Mungu wenu amewabariki.
8 [j]Msifanye kama tunavyofanya hapa
leo, kila mtu anavyopenda mwenyewe,
9 [k]kwa kuwa bado hamjafikia mahali pa
mapumziko na urithi ambao BWANA
Mungu wenu anawapa. 10 [l]Lakini mtavuka
Yordani na kuishi katika nchi BWANA
Mungu wenu anayowapa kama urithi,
naye atawapa pumziko kutokana na adui
zenu wote wanaowazunguka ili ninyi mpate
kuishi kwa salama. 11 [m]Kisha kuhusu mahali
BWANA Mungu wenu atakapopachagua
kuwa mahali pa makao ya Jina lake,
hapo ndipo inapowapasa kuleta kila
kitu ninachowaamuru: sadaka zenu za
kuteketezwa na dhabihu, zaka zenu na
changizo, pamoja na vitu vyote vyenye
thamani ambavyo mmeweka nadhiri
kumtolea BWANA. 12 [n]Hapo furahini mbele
za BWANA Mungu wenu, ninyi, wana wenu
na binti zenu, watumishi wenu wa kiume
na wa kike, pamoja na Walawi kutoka miji
yenu ambao hawana mgawo wala urithi
wao wenyewe. 13 [o]Kuweni waangalifu,
msitoe dhabihu zenu za kuteketezwa
mahali popote mnapopapenda. 14 Mtazitoa
tu mahali pale ambapo BWANA atachagua

---

[a]**11:30** Mwa 12:6; Yos 4:19; 5:9; 9:6; 10:6; 14:6; 15:7; Amu 2:1; 2Fal 2:1; Mik 6:5; Hes 33:53; Kum 12:10; Yos 1:11; 11:23
[b]**11:31** Kum 28:1-14; Za 24:5
[c]**12:1** Za 119:5; Kum 4:9-10; 6:15; 1Fal 8:40; Eze 20:19; Gal 6:9
[d]**12:2** Hes 21:28; 1Fal 14:23; 2Fal 17:10; Isa 57:5; Yer 2:20; 3:6-13; Kut 34:33
[e]**12:3** 2Fal 11:8; Kut 32:20; 34:13; 1Fal 14:15; Hes 33:53; Kut 23:13; Amu 2:2; Za 16:4; Zek 13:2
[f]**12:4** 2Fal 17:15; Yer 10:2
[g]**12:5** Kut 20:24; 2Sam 7:13; Kum 14:23; 15:20; 16:2, 11; 18:6; 26:2; 1Sam 2:29; 1Fal 1:5; 5; 8:16; 9:3; 2Nya 2:4; 6:6; 7:12-16; Ezr 6:12; 7:15; Za 26:8; 78:68; Zek 2:12
[h]**12:6** Law 27:30; Mwa 28:20; Yos 22:27; Isa 66:20; Kum 14:22
[i]**12:7** Kut 18:12; Mhu 3:12-13; Law 23:40; Isa 62:9
[j]**12:8** Amu 17:6; 21:25
[k]**12:9** Kut 33:14; Kum 3:20; Za 95:11; Mik 2:10; Kum 4:21
[l]**12:10** Kum 11:31; Kut 33:14; Law 1:3; Yos 22:23
[m]**12:11** Kum 14:23; 15:20; 16:2; Yos 18:1; 1Fal 8:29; Za 78:68; 87:2
[n]**12:12** Kum 26:11-13; 18:20; 9:10; 10:9; 14:29
[o]**12:13** Law 17:4

katika mojawapo ya makabila yenu, nanyi hapo zingatieni kila jambo ninalowaamuru.

15 [a]Hata hivyo, mnaweza kuwachinja wanyama wenu katika miji yenu yoyote ile na kula nyama nyingi mpendavyo kama vile mmemchinja paa au kulungu, kulingana na baraka mtakazojaliwa na BWANA Mungu wenu. Watu walio najisi au walio safi wanaweza kula. 16 [b]Lakini kamwe usinywe damu; imwage juu ya ardhi kama maji. 17 [c]Hamruhusiwi kula katika miji yenu zaka yenu ya nafaka, ya divai mpya na ya mafuta, au mzaliwa wa kwanza wa makundi yenu ya ng'ombe na makundi yenu ya mbuzi na kondoo, wala chochote ambacho mmeweka nadhiri kukitoa, au sadaka zako za hiari, wala matoleo maalum. 18 [d]Badala yake, mtakula vitu hivyo katika uwepo wa BWANA Mungu wenu mahali ambapo BWANA Mungu wenu atapachagua: wewe, wana wako na binti zako, watumishi wako wa kiume na wa kike, na Walawi kutoka miji yenu. Mnatakiwa mfurahi mbele za BWANA Mungu wenu kwa kula kitu mtakachoweka mikono yenu. 19 [e]Mwe waangalifu msiwapuuze Walawi kwa muda wote mnaoishi katika nchi yenu.

20 [f]BWANA Mungu wenu atakapokuwa ameongeza nchi yenu kama alivyowaahidi, nanyi mkitamani nyama na mkisema, "Ningependa nyama," hapo unaweza kula nyingi upendavyo. 21 [g]Kama mahali ambapo BWANA Mungu wenu atapachagua kuweka Jina lake ni mbali sana kutoka kwenu, unaweza kuchinja wanyama kutoka makundi yenu ya ng'ombe, ya mbuzi na ya kondoo ambayo BWANA amewapa, kama nilivyokuamuru, na mkiwa katika miji yenu wenyewe mnaweza kula nyingi mtakavyo. 22 Mle kama vile mngekula paa na kulungu. Wote walio najisi kiibada na walio safi mwaweza kula. 23 [h]Lakini hakikisheni kwamba hamkunywa damu, kwa sababu damu ni uhai, kamwe msile uhai pamoja na nyama. 24 Hamruhusiwi kamwe kunywa damu; imwageni juu ya ardhi kama maji. 25 [i]Msinywe damu, ili mweze kufanikiwa ninyi pamoja na watoto wenu baada yenu, kwa sababu mtakuwa mkifanya lililo haki machoni pa BWANA.

26 [j]Lakini vichukueni vitu vyenu vilivyowekwa wakfu pamoja na vile mlivyoweka nadhiri, mwende mahali pale BWANA atakapopachagua. 27 [k]Leteni sadaka zenu za kuteketezwa juu ya madhabahu ya BWANA Mungu wenu, vyote nyama na damu. Damu ya dhabihu zenu lazima imiminwe kando ya madhabahu ya BWANA Mungu wenu, lakini nyama mnaweza kula. 28 [l]Mwe waangalifu kutii masharti haya yote ninayowapa, ili kwamba siku zote mweze kufanikiwa, ninyi pamoja na watoto wenu baada yenu, kwa sababu mtakuwa mkifanya lililo jema na sahihi mbele za macho ya BWANA Mungu wenu.

29 [m]BWANA Mungu wenu atayakatilia mbali mbele yenu mataifa ambayo punde kidogo mtayavamia na kuyaondoa. Lakini mtakapokuwa mmeyafukuza na kuishi katika nchi yao, 30 [n]na baada ya kuangamizwa mbele yenu, mwe waangalifu msijiingize katika tanzi kwa kuuliza habari za miungu yao, mkisema, "Je, mataifa haya hutumikiaje miungu yao? Nasi tutafanya vivyo hivyo." 31 [o]Kamwe msimwabudu BWANA Mungu wenu kwa njia wanayoabudu miungu yao, kwa sababu

[a]**12:15** Kum 14:5; 15:22; Mwa 9:3
[b]**12:16** Mwa 9:4; Mdo 15:20; Mwa 35:14; 1Nya 11:18; Yer 7:18; Law 17:13; Kum 15:23; Yn 19:34; Law 7:26
[c]**12:17** Law 27:30; Hes 18:12-19; Kum 14:23; 15:20
[d]**12:18** Kum 14:23; 15:20; 14:26; Neh 8:10; Mhu 3:12-13; 5:18-20
[e]**12:19** Kum 14:27; Neh 13:10; Mal 3:8
[f]**12:20** Kut 34:24; Mwa 15:8, 18; Kum 11:24; Kut 16:3
[g]**12:21** Kum 14:24; Law 17:4
[h]**12:23** Law 7:26; Eze 33:25; Mwa 9:4; Law 17:11, 14
[i]**12:25** Kum 4:40; Kut 15:26; Kum 13:18; 1Fal 11:38; 2Fal 12:2; Isa 3:10
[j]**12:26** Hes 5:9-10; 18:19
[k]**12:27** Law 1:13; 3:1-17
[l]**12:28** Kum 4:40; Mhu 8:12; Za 25:12, 13; Mit 1:33; 3:1-4
[m]**12:29** Yos 23:4; Kum 6:10; Kut 23:23; Yos 23:4; Za 78:55
[n]**12:30** Kut 10:7
[o]**12:31** Law 18:25; 2Fal 3:27; Kum 9:5; Yer 32:35; 2Fal 17:15; 2Nya 33:2; 36:14

katika kuabudu miungu yao, wanafanya
aina zote za machukizo anayoyachukia
Bwana. Hata huwateketeza wana wao
na binti zao kwa moto kama kafara kwa
miungu yao.
32 [a]Angalieni kwamba mnafanya yote
niliyowaamuru; msiongeze kitu wala
msipunguze kitu.

*Kuabudu Miungu Mingine*

13 [b]Kama nabii, au yule anayetabiri kwa
njia ya ndoto, akijitokeza miongoni
mwenu na akawatangazia ishara ya
miujiza na ajabu, 2 [c]ikiwa ishara au ajabu
ya aliyozungumza ikatokea, naye akasema,
“Na tufuate miungu mingine” (miungu
ambayo hamjaifahamu) “na tuiabudu,”
3 [d]kamwe msiyasikilize maneno ya nabii
wala mwota ndoto huyo. Bwana Mungu
wenu anawajaribu kuangalia kama
mnampenda kwa moyo wenu wote na
kwa roho yenu yote. 4 [e]Ni Bwana Mungu
wenu ambaye mnapaswa kumfuata tena
ni yeye mnapaswa kumheshimu. Shikeni
maagizo yake na kumtii, mtumikieni na
kushikamana naye. 5 [f]Huyo nabii au mwota
ndoto lazima auawe, kwa sababu amehubiri
uasi dhidi ya Bwana Mungu wenu,
ambaye aliwatoa kutoka nchi ya Misri
na kuwakomboa kutoka nchi ya utumwa;
amejaribu kuwageuza kutoka njia ambayo
Bwana Mungu wenu aliwaagiza mfuate. Ni
lazima mwondoe uovu miongoni mwenu.
6 [g]Kama ndugu yako hasa, au mwanao au
binti yako, au mke umpendaye, au rafiki
yako wa karibu sana akikushawishi kwa siri,
akisema, “Na twende tukaabudu miungu
mingine” (miungu ambayo ninyi wala baba
zenu hamkuifahamu, 7 miungu ya watu
wanaowazunguka, ikiwa karibu au mbali,
kutoka mwisho mmoja wa nchi mpaka
mwingine), 8 [h]usikubali wala usimsikilize.
Usimhurumie! Usimwache wala usimkinge.
9 [i]Hakika ni lazima auawe. Ni lazima mkono
wako uwe wa kwanza katika kumuua kisha
mikono ya watu wengine wote. 10 [j]Mpigeni
kwa mawe mpaka afe, kwa sababu alijaribu
kuwageuza mtoke kwa Bwana Mungu
wenu ambaye aliwatoa Misri, kutoka nchi
ya utumwa. 11 [k]Kisha Israeli wote watasikia
na kuogopa, wala hakuna mmoja miongoni
mwenu atakayefanya uovu tena.
12 [l]Kama mkisikia ikisemwa kwamba
moja ya miji ambayo Bwana Mungu
wenu anawapa mkae ndani yake 13 [m]kuna
wanaume waovu wameinuka miongoni
mwenu na wamewapotosha watu wa mji,
wakisema, “Twendeni tukaabudu miungu
mingine” (miungu ambayo hamkuifahamu),
14 [n]ndipo itakubidi kuuliza, kupima na
kuchunguza kwa makini. Kama ni kweli,
tena ikihakikishwa kwamba jambo hili
lichukizalo limefanyika miongoni mwenu,
15 [o]kwa hakika ni lazima mwaue kwa
upanga wale wote wanaoishi katika mji ule.
Uharibuni kabisa, pamoja na watu wake na
mifugo yake. 16 [p]Kusanyeni nyara zote za
mji katika uwanja wa wazi na kuuchoma
mji kabisa pamoja na nyara zake zote
kama sadaka ya kuteketezwa kwa Bwana
Mungu wenu. Utabaki kuwa magofu milele

[a]**12:32** Kum 4:2; Ufu 22:18-19; Yos 1:7; Mit 30:6
[b]**13:1** Mt 24:24; Mk 13:22; 2The 2:9; Mwa 20:3; Yer 23:25; 27:9; 29:8
[c]**13:2** Kum 11:28; 18:22; 1Sam 2:34; 10:9; 2Fal 19:29; 20:9; Isa 7:11; Kum 11:28
[d]**13:3** 2Pet 2:1; 1Sam 28:6; Mwa 22:1; 1Fal 13:18; 22:23; Yer 29:31; 43:2; Eze 13:9; 1Kor 11:19; Kum 6:5
[e]**13:4** 2Fal 23:8; 2Nya 34:31; 2Yn 6; Kum 6:13; 10:20; Za 5:7
[f]**13:5** Kut 21:12; 22:20; Kum 4:19; 17:7-12; 19:19; 24:7; Amu 20:13; 1Kor 5:13
[g]**13:6** Kum 17:2-7; 29:18; 11:28
[h]**13:8** Mit 1:10; Kum 7:2; Kut 20:3; Gal 1:8-9; 1Yn 5:21
[i]**13:9** Law 24:14; Kum 17:5-7; Mdo 7:58
[j]**13:10** Kut 20:3
[k]**13:11** Kum 17:13; 19:20; 21:21; 1Tim 5:20
[l]**13:12** Yos 22:11; Amu 20:1
[m]**13:13** Amu 19:22; 20:13; 1Sam 2:12; 10:27; 25:17; 1Fal 21:10; 1Yn 2:19
[n]**13:14** Amu 20:12; Kum 17:4
[o]**13:15** Isa 24:6; 34:5; 43:28; 47:6; Mao 2:6; Dan 9:11; Zek 8:13; Mal 4:6; Kut 22:20
[p]**13:16** 2Fal 25:9; Yer 39:9; 52:13; Eze 16:41; Kum 7:25-26; Yos 6:24; 8:28; Isa 7:16; 17:1; 24:10; 25:2; 27:10; 32:14-19; 37:26; Yer 49:2; Mik 1:6

na hautajengwa tena. [17] [a]Hakuna kimoja
kati ya vitu vilivyolaaniwa kitakachokutwa
mikononi mwenu, ili BWANA ageuze hasira
yake kali. Atawahurumia na kuwa na
rehema kwenu pia kuongeza idadi yenu,
kama alivyowaahidi baba zenu, [18] [b]kwa
sababu mnamtii BWANA Mungu wenu,
mkizishika amri zake zote zile ninazowapa
leo na kufanya lile lililo jema machoni pake.

*Vyakula Vilivyo Najisi Na Vilivyo Safi*

**(Walawi 11:1-47)**

14 [c]Ninyi ni watoto wa BWANA Mungu
wenu. Msijichanje ama kujinyoa
upara kwenye paji la uso kwa ajili ya
aliyekufa, [2] [de]kwa maana ninyi ni taifa
takatifu kwa BWANA Mungu wenu. BWANA
amewachagua ninyi kuwa taifa la kipekee
kutoka mataifa yote juu ya uso wa dunia,
mwe tunu yake.

[3] [f]Msile kitu chochote ambacho ni
machukizo. [4] [g]Hawa ndio wanyama
mtakaokula: ng'ombe, kondoo, mbuzi,
[5] [h]kulungu, paa, kongoni, paa mweupe,
mbuzi-mwitu, pofu na kondoo wa mlimani.
[6] Mnaweza kumla mnyama yeyote mwenye
kwato zilizogawanyika mara mbili, pia yule
anayecheua. [7] Hata hivyo, miongoni mwa
wale wanaocheua au wale walio na kwato
zilizogawanyika kamwe msile ngamia,
sungura na pelele. Iwapo wanacheua,
lakini hawana kwato zilizogawanyika;
ni najisi kwenu kwa taratibu za kiibada.
[8] [i]Nguruwe pia ni najisi; ingawa ana kwato
zilizogawanyika, hacheui. Msile nyama
yake wala kugusa mzoga wake.

[9] Katika viumbe hai vyote viishivyo
kwenye maji, mnaweza kula yeyote aliye
na mapezi na magamba. [10] Lakini chochote
kisicho na mapezi na magamba msile;
kwenu ni najisi.

[11] Mnaweza kula ndege yeyote aliye safi.
[12] [j]Lakini wafuatao msiwale: tai, furukombe,
kipungu, [13] [k]kengewa mwekundu, kengewa
mweusi, mwewe wa aina yoyote, [14] [l]kunguru
wa aina yoyote, [15] mbuni, kiruka-njia,
dudumizi, kipanga wa aina yoyote, [16] bundi,
mumbi, bundi mkubwa, [17] [m]mwari, nderi,
mnandi, [18] korongo, koikoi wa aina yoyote,
hudihudi na popo.

[19] Wadudu wote warukao kwa makundi
ni najisi kwenu, msiwale. [20] [n]Lakini viumbe
vyote vyenye mabawa vilivyo safi mwaweza
kula.

[21] [o]Msile kitu chochote mtakachokuta
kimekufa. Mnaweza kumpa mgeni yeyote
anayeishi katika mojawapo ya miji yenu,
naye anaweza kula au mnaweza kumuuzia
mtu wa nchi nyingine. Lakini ninyi ni watu
watakatifu kwa BWANA Mungu wenu.

Msitokose mwana-mbuzi katika maziwa
ya mama yake.

*Zaka*

[22] [p]Hakikisheni mmetenga sehemu ya
kumi ya mazao yote ya mashamba yenu
kila mwaka. [23] [q]Mtakula zaka za nafaka
yenu, divai mpya, mafuta na wazaliwa wa
kwanza wa makundi yenu ya ng'ombe na ya
kondoo na mbuzi mbele za BWANA Mungu
wenu pale mahali atakapopachagua kama
maskani kwa ajili ya Jina lake, ili kwamba
mpate kujifunza kumheshimu BWANA

---

[a]**13:17** Kut 30:12; Mwa 12:2; 13:14; 26:24; 28:14; 43:14; Hes 25:4; Kum 30:3; 7:13
[b]**13:18** Kum 12:25-28; 12:25-28; Mt 6:33; 7:21-24
[c]**14:1** Yn 1:12; Rum 8:14; 9:8; Yer 16:6; Mwa 6:2-4; Kut 4:22-23; Gal 3:26; 1The 4:13
[d]**14:2** Mwa 28:14; Kut 8:22; 22:31; Isa 6:13; Mt 2:15; Law 20:26; Rum 12:1; Kum 7:6; 26:18-19
[e]**14:2** Kut 19:5; 2Sam 7:23, 24
[f]**14:3** Eze 4:14; Isa 65:4; Mdo 10:13; Rum 14:14
[g]**14:4** Mdo 10:14; Law 7:23; 11:2-45
[h]**14:5** Kum 12:15; Ay 39:1; Za 104:18
[i]**14:8** Law 5:12; 11:26-27
[j]**14:12** Law 11:13
[k]**14:13** Mwa 2:11; Isa 34:15
[l]**14:14** Mwa 8:17
[m]**14:17** Za 102:6; Isa 13:21; 14:23; 34:11; Sef 2:14
[n]**14:20** Law 20:25
[o]**14:21** Law 11:39; 14:2; 17:15; Kut 23:19; 22:31; Law 22:8; Eze 44:31
[p]**14:22** Mwa 14:20; Law 27:30; Hes 18:21; Neh 10:37; Kum 12:6, 17
[q]**14:23** Kum 12:5, 17, 18; Za 4:7; 1Fal 3:2; Kum 4:10; Za 22:23; 33:8; Mal 2:5; Mit 3:13; Isa 8:13; Yer 32:38-41; Ebr 12:28

Mungu wenu daima. 24 [a]Lakini ikiwa mahali
pale ni mbali sana nanyi mmebarikiwa na
BWANA Mungu wenu na hamwezi kubeba
zaka yenu (kwa sababu mahali pale BWANA
atakapopachagua kuliweka Jina lake
ni mbali sana), 25 [b]basi badilisheni zaka
yenu kuwa fedha, mkaichukue hiyo fedha
mwende nayo mahali BWANA Mungu wenu
atakapopachagua. 26 [c]Tumieni hiyo fedha
kununua chochote ukitakacho: ng'ombe,
kondoo, divai au kinywaji chochote chenye
chachu au chochote mnachotaka. Kisha
ninyi na wa nyumbani mwenu mtaila
mbele za BWANA Mungu wenu na kufurahi.
27 [d]Msiache kuwajali Walawi waishio katika
miji yenu, kwa kuwa hao hawana shamba
wala urithi wao wenyewe.

28 [e]Mwishoni mwa kila mwaka wa tatu,
leteni zaka zote za mazao ya miaka ile na
uyahifadhi kwenye miji yenu, 29 [f]ili Walawi
(ambao hawana mashamba wala urithi wao
wenyewe) na wageni, yatima na wajane
wanaoishi kwenye miji yenu wapate kuja
kula na kushiba, ili BWANA Mungu wenu
apate kuwabariki ninyi katika kazi zote za
mikono yenu.

*Mwaka Wa Kufuta Madeni*

**(Walawi 25:1-7)**

15 [g]Kila mwisho wa miaka saba ni
lazima mfute madeni. 2 Hivi ndivyo
itakavyofanyika: Kila mkopeshaji atafuta
mkopo aliomkopesha Mwisraeli mwenzake.
Hatamtaka Mwisraeli mwenzake au
ndugu yake amlipe hilo deni, kwa sababu
wakati wa BWANA wa kufuta madeni
umetangazwa. 3 [h]Unaweza kudai malipo
kwa mgeni, lakini lazima ufute kila deni
ambalo unamdai ndugu yako. 4 [i]Hata hivyo,
hapatakuwepo maskini miongoni mwenu,
kwa kuwa katika nchi BWANA Mungu
wenu anayowapa kuimiliki kama urithi
wenu, atawabariki sana, 5 [j]ikiwa tutamtii
BWANA Mungu wenu kikamilifu na kuwa
waangalifu kuyafuata maagizo haya yote
ninayowapa leo. 6 [k]Kwa kuwa BWANA
Mungu wenu atawabariki kama alivyoahidi,
nanyi mtawakopesha mataifa mengi lakini
hamtakopa kwa yeyote. Mtatawala mataifa
mengi lakini hakuna taifa litakalowatawala
ninyi.

7 [l]Ikiwa kuna mtu maskini miongoni
mwa ndugu zenu, katika mji wowote wa
hiyo nchi ambayo BWANA Mungu wenu
anawapa, msiwe na moyo mgumu wala
usimfumbie mkono ndugu yako aliye
maskini. 8 [m]Afadhali fungua mikono yako na
umkopeshe kwa hiari chochote anachohitaji.
9 [n]Jihadhari usijiwekee wazo hili ovu:
"Mwaka wa saba, mwaka wa kufuta madeni
umekaribia," usije ukaonyesha nia mbaya
kwa ndugu yako mhitaji na ukaacha kumpa
chochote. Anaweza kumlalamikia BWANA
dhidi yako nawe utakuwa umepatikana na
hatia ya dhambi. 10 [o]Mpe kwa ukarimu na
ufanye hivyo bila kinyongo moyoni, ndipo
kwa sababu ya hili BWANA Mungu wenu
atakubariki katika kazi zako zote na kwa
kila kitu utakachokiwekea mkono wako.
11 [p]Siku zote watakuwepo watu maskini
katika nchi. Kwa hiyo ninawaamuru mwe
na mikono iliyokunjuliwa kuwaelekea
ndugu zenu, kuwaelekea maskini na
wahitaji katika nchi yenu.

---

[a]**14:24** Kum 12:21
[b]**14:25** Mt 21:12; Yn 2:14
[c]**14:26** Law 10:9; 23:40; Mhu 10:16-17; Kum 12:7-8
[d]**14:27** Kum 12:19; Hes 18:20; 26:62; Kum 18:1-2; Rum 13:4; 15:27; 1Kor 9:1-14
[e]**14:28** Law 27:30; Kum 26:12
[f]**14:29** Mwa 47:22; Hes 26:62; Kum 16:11; 24:19-21; Za 94:6; Isa 1:17; 58:6; Kum 6:11; 15:10; Za 41:1; Mit 22:9; Mt 3:10; Kum 10:18; Eze 22:7, 29; Lk 14:12; Ebr 13:2; Mal 3:10; Lk 11:41; 2Kor 9:6-11
[g]**15:1** Kum 31:10; Neh 10:31; Kut 23:10; Yer 34:14
[h]**15:3** Mwa 31:15; Kum 23:20; 28:12; Rut 2:10
[i]**15:4** Kum 28:5, 8
[j]**15:5** Kut 15:26; Kum 7:12; 28:1
[k]**15:6** Kum 28:12-13, 44; Mit 22:7
[l]**15:7** Mt 26:11; 18:30; 1Yn 3:17
[m]**15:8** Mt 5:42; Lk 6:34; Mdo 24:17; Law 25:35; Gal 2:10
[n]**15:9** Mt 20:15; Kut 22:23; Ay 5:15; Yak 5:4; Amo 5:11; Mit 28:22; Za 140:12
[o]**15:10** 2Kor 9:5; Kum 14:29; 24:19; Mt 25:40; Mdo 20:35; Rum 12:8; 1Tim 6:18; 1Pet 4:11
[p]**15:11** Mt 26:11; Mk 14:7; Yn 12:8

*Kuwaacha Huru Watumwa*

**(Kutoka 21:1-18)**

12 [a]Kama Mwebrania mwenzako,
mwanaume au mwanamke, akijiuza
kwako na kukutumikia miaka sita, katika
mwaka wa saba ni lazima umwache
aende zake akiwa huru. 13 Nawe wakati
utakapomwachia usimwache aende
mikono mitupu. 14 [b]Mpe kwa uhuru kutoka
zizi lako la kondoo na mbuzi, kutoka
sakafu yako ya kupuria nafaka na kutoka
mashinikizo yako ya kukamulia divai. Mpe
kama vile ambavyo BWANA Mungu wako
alivyokubariki. 15 [c]Kumbukeni kuwa ninyi
mlikuwa watumwa huko Misri naye BWANA
Mungu wenu aliwakomboa. Ndiyo sababu
nimewapa agizo hili leo.

16 [d]Lakini mtumishi wako akikuambia,
"Sitaki kukuacha," kwa sababu anakupenda
wewe na jamaa yako naye anaridhika nawe,
17 ndipo utachukua chuma kidogo utoboe
sikio lake mpaka hicho chuma kiingie
kwenye ubao wa mlango, naye atakuwa
mtumishi wako wa maisha. Ufanye vivyo
hivyo kwa mtumishi wa kike.

18 [e]Usifikiri kuwa kuna ugumu kumwacha
mtumishi wako huru, kwa sababu utumishi
wake kwako kwa miaka hii sita umekuwa wa
thamani mara mbili ya ujira wa mtumishi
wa kuajiriwa. Naye BWANA Mungu wenu
atakubarikia kwa kila kitu utakachofanya.

*Wazaliwa Wa Kwanza Wa Wanyama*

19 [f]Wekeni wakfu kwa BWANA Mungu
wenu kila mzaliwa wa kwanza wa kiume wa
makundi yenu ya ng'ombe na ya mbuzi na
kondoo. Maksai walio wazaliwa wa kwanza
msiwafanyize kazi, wala msinyoe manyoya
ya wazaliwa wa kwanza wa kondoo. 20 [g]Kila
mwaka ninyi na jamaa zenu mtapaswa
kuwala mbele za BWANA Mungu wenu
pale mahali atakapopachagua. 21 [h]Kama
mnyama ana dosari, akiwa ni kilema au
kipofu au kama ana kilema kibaya, kamwe
usimtoe dhabihu kwa BWANA Mungu wenu.
22 [i]Itawapasa kumla ninyi wenyewe katika
miji yenu. Wote wasio safi na walio safi
kwa desturi za kiibada mwaweza kula kama
vile mnavyokula paa au kulungu. 23 [j]Lakini
kamwe msinywe damu; imwageni ardhini
kama maji.

*Pasaka*

**(Kutoka 12:1-20)**

16 [k]Shikeni mwezi wa Abibu, na
kuiadhimisha Pasaka ya BWANA
Mungu wenu, kwa sababu katika mwezi
wa Abibu, Mungu aliwatoa Misri usiku.
2 [l]Mtatoa dhabihu ya Pasaka ya mnyama
kwa BWANA Mungu wenu kutoka kundi
lenu la mbuzi na kondoo au la ng'ombe,
mahali pale ambapo BWANA atapachagua
kama makao kwa ajili ya Jina lake. 3 [m]Msile
nyama hiyo pamoja na mikate iliyotiwa
chachu, lakini kwa siku saba mtakula
mikate isiyotiwa chachu, mikate ya kujitesa,
kwa sababu mliondoka Misri kwa haraka,
ili kwamba siku zote za maisha yenu mpate
kukumbuka wakati wenu wa kuondoka
Misri. 4 [n]Chachu isionekane katika mali
zenu katika nchi yenu yote kwa siku saba.
Nyama yoyote ya dhabihu mtakayotoa
jioni ya siku ya kwanza isibakizwe mpaka
asubuhi.

5 Kamwe msitoe dhabihu ya Pasaka
katika mji wowote ambao BWANA Mungu
wenu amewapa, 6 [o]isipokuwa mahali

---

[a]**15:12** Yer 34:14; Kut 21:2; Law 25:39
[b]**15:14** Hes 18:27; Mit 10:22
[c]**15:15** Kut 13:3; Yer 34:13; Kut 20:2; Kum 4:34; 9:26; 16:12; 24:18; Yer 16:14; 27:7
[d]**15:16** Kum 21:5-6
[e]**15:18** Isa 16:14; 21:16
[f]**15:19** Law 27:9; Kut 13:2; Mwa 4:4; Kut 22:30
[g]**15:20** Law 7:15-18; Kum 12:5-7; 14:23
[h]**15:21** Kut 12:5; Law 22:19-25; Kum 17:1; Mal 1:8, 13
[i]**15:22** Kum 12:15, 22
[j]**15:23** Mwa 9:4; Kum 12:16; Eze 33:25; Law 7:26; 17:10
[k]**16:1** Kut 12:2; 12:11; 2Fal 23:21; Mt 26:17-29; Kut 13:4; Law 23:5; Hes 9:2-5; Yn 18:28; 1Kor 5:7, 8; Ebr 11:28; 1Kor 5:7, 8; Ebr 11:28
[l]**16:2** Kum 12:5, 26
[m]**16:3** Kut 12:15-20, 39; 34:18; 1Kor 5:8; Kut 12:11; Kum 4:9; Kut 13:3, 6-7; Hes 28:19; 2Nya 35:7; Mt 26:2
[n]**16:4** Kut 12:6; 12:8; Mk 14:12; Kut 12:10
[o]**16:6** Kut 12:42; Kum 12:5; Mt 27:46

atakapopachagua kama makao kwa ajili
ya Jina lake. Hapo ndipo lazima mtoe
dhabihu ya Pasaka jioni, jua litakapotua,
iwe kumbukumbu yenu ya kutoka Misri.
7 [a]Okeni na mle mahali pale ambapo
BWANA Mungu wenu atakapopachagua,
kisha asubuhi mrudi kwenye mahema yenu.
8 [b]Kwa siku sita mtakula mikate isiyotiwa
chachu na siku ya saba fanyeni kusanyiko
kwa ajili ya BWANA Mungu wenu na
msifanye kazi.

*Sikukuu Ya Mavuno*

**(Kutoka 34:22; Walawi 23:15-21)**

9 [c]Mhesabu majuma saba tangu wakati
mnapoanza kuchukua mundu kuvuna
nafaka. 10 [d]Kisha msherehekee Sikukuu ya
Majuma kwa BWANA Mungu wenu kwa
kutoa sadaka ya hiari kwa kadiri ya baraka
ambayo BWANA Mungu wenu amewapa.
11 [e]Shangilieni mbele za BWANA Mungu
wenu mahali atakapopachagua kama
makao ya Jina lake, ninyi, wana wenu na
binti zenu, watumishi wenu wa kiume na
wa kike, Walawi walio katika miji yenu,
na wageni, yatima na wajane waishio
miongoni mwenu. 12 [f]Kumbukeni kwamba
mlikuwa watumwa kule Misri na mfuate
amri hizi kwa uangalifu.

*Sikukuu Ya Vibanda*

**(Walawi 23:33-43)**

13 [g][h]Adhimisheni sikukuu ya vibanda kwa
siku saba baada ya kukusanya mazao yenu
ya nafaka na kukamua zabibu. 14 [i]Mfurahie
sikukuu yenu, ninyi, wana wenu, binti zenu,
watumishi wenu wa kiume na wa kike,
Walawi, wageni, yatima na wajane ambao
wanaishi katika miji yenu. 15 [j]Kwa siku saba
mtaiadhimisha sikukuu ya BWANA Mungu
wenu katika mahali atakapopachagua
BWANA. Kwa kuwa BWANA Mungu wenu
atawabariki katika mavuno yenu na katika
kazi zote za mikono yenu na furaha yenu
itakamilika.

16 [k]Wanaume wenu wote lazima wajitokeze
mara tatu kwa mwaka mbele za BWANA
Mungu wenu mahali atakapopachagua:
kwa ajili ya Sikukuu ya Mikate Isiyotiwa
Chachu, Sikukuu ya Majuma, na Sikukuu
ya Vibanda. Hakuna mtu atakayejitokeza
mbele za BWANA mikono mitupu: 17 [l]Kila
mmoja wenu ni lazima alete zawadi
kulingana na jinsi ambavyo BWANA Mungu
wenu alivyowabariki.

*Waamuzi*

18 [m]Wateue waamuzi na maafisa kwa kila
kabila lenu katika kila mji ambao BWANA
Mungu wenu anawapa, nao watawaamua
watu kwa usawa. 19 [n]Msipotoshe haki wala
msifanye upendeleo. Msikubali rushwa kwa
sababu rushwa hupofusha macho ya wenye
busara na kugeuza maneno ya wenye haki.
20 [o]Mfuate haki na haki peke yake, ili mweze
kuishi na kuimiliki nchi ambayo BWANA
Mungu wenu anawapa.

*Kuabudu Miungu Mingine*

21 [p]Msisimamishe nguzo yoyote ya Ashera
kando ya madhabahu mliyomjengea BWANA

[a]**16:7** Kut 12:8; 2Nya 35:13; 2Fal 23:23; Yn 2:13; 11:55
[b]**16:8** Law 23:8; Mt 26:17; Lk 2:41; 22:7; Yn 2:13; Kut 12:16
[c]**16:9** Mdo 2:1; Kut 23:16; 34:22; Hes 28:26; Law 23:15
[d]**16:10** Mt 10:22; Yoe 2:14; 1Kor 16:2
[e]**16:11** Kum 12:7; Kut 20:24; 2Sam 7:13; Kum 12:12; 14:29; Neh 8:10; Lk 14:12
[f]**16:12** Kum 15:15
[g]**16:13** Law 2:14; Mwa 2:14; 27:37; Kut 23:16; Law 23:34; Mwa 15:13; Kut 1:11, 14; Za 105:23, 25
[h]**16:13** Kut 23:16; Law 23:34; Hes 29:12
[i]**16:14** Kum 26:11; Neh 8:9; Mhu 9:7; 1Sam 12:1-6; 25:6-8
[j]**16:15** Ay 38:7; Za 4:7; 28:7; 30:11; Law 23:39
[k]**16:16** Kum 31:11; Za 84:7; Kut 12:17; 23:14, 16; Ezr 3:4; Kut 34:20
[l]**16:17** 2Kor 8:12
[m]**16:18** Kut 18:21, 26; Mwa 31:37; Kum 1:16
[n]**16:19** Kut 23:2, 8; Law 19:15; Kut 18:21; 1Sam 8:3; Kum 1:17; Mhu 7:7; Ay 31:21, 22; Mit 17:23; 24:23; Isa 1:17, 23; Mdo 10:34
[o]**16:20** Kum 4:1
[p]**16:21** Kum 7:5; Kut 34:13; 1Fal 14:15; 2Fal 17:16; 21:3; 2Nya 33:3; Kut 34:13; Amu 3:7

Mungu wenu, 22 [a]wala msisimamishe jiwe la
kuabudu, kwa maana BWANA Mungu wenu
anavichukia vitu hivi.

17 [b]Msimtolee BWANA Mungu wenu
dhabihu ya maksai au kondoo ambaye
ana dosari yoyote au hitilafu ndani yake,
kwa kuwa hilo litakuwa chukizo kwake.

2 [c]Ikiwa mwanaume au mwanamke
anayeishi kati ya mojawapo ya miji akupayo
BWANA, anakutwa anafanya uovu mbele
za BWANA Mungu wenu, kwa kuvunja
Agano lake, 3 [d]naye amekwenda kinyume
na agizo langu kuabudu miungu mingine na
kuisujudia, kama vile jua, mwezi au nyota
za angani, 4 [e]hili likiwa limeletwa mbele
yenu, ni lazima kulichunguza kikamilifu.
Ikiwa ni kweli na kuwa limehakikishwa
kwamba hili ni chukizo lililofanyika katika
Israeli, 5 [f]mchukueni huyo mwanaume au
mwanamke ambaye amelifanya tendo
hili ovu kwenye lango la mji wenu na
kumpiga mawe mtu huyo mpaka afe.
6 [gh]Kwa ushuhuda wa mashahidi wawili au
watatu mtu huyo atauawa, bali hakuna mtu
atakayeuawa kwa ushuhuda wa shahidi
mmoja tu. 7 [i]Ni lazima kwanza mikono ya
mashahidi itangulie kumuua huyo mtu,
kisha mikono ya watu wote. Ni lazima
mwondoe uovu miongoni mwenu.

### *Mahakama Za Sheria*

8 [j]Kama mashauri yanaletwa katika
mahakama zenu ambayo ni magumu zaidi
kwenu kuyaamua, ikiwa ni umwagaji wa
damu, madai au mashambulio, yapelekeni
mahali ambapo BWANA Mungu wenu
atapachagua. 9 [k]Nendeni kwa makuhani,
ambao ni Walawi, na kwa mwamuzi ambaye
atakuwa kazini wakati huo. Ulizeni kwao
nao watawapa maamuzi. 10 Ni lazima mtende
sawasawa na maamuzi watakayowapa
mahali BWANA atakapopachagua.
Kuweni waangalifu kufanya kila kitu
watakachowaongoza kufanya. 11 [l]Fanyeni
sawasawa na sheria wanayowafundisha na
maamuzi wanayowapa. Msigeuke mkono
wa kuume au kushoto kuacha kufanya
yale wanayowaambia. 12 [m]Mwanaume
atakayeonyesha dharau kwa mwamuzi au
kwa kuhani ambaye amewekwa kumtumikia
BWANA Mungu wenu lazima auawe. Lazima
mwondoe uovu katika Israeli. 13 [n]Watu wote
watasikia na kuogopa, nao hawatakuwa
wenye kudharau tena.

### *Mfalme*

14 [o]Wakati utakapoingia katika nchi
anayowapa BWANA Mungu wenu kuimiliki
na kukaa humo, nanyi mkasema, “Na
tumweke mfalme juu yetu kama mataifa
yanayotuzunguka,” 15 [p]kuweni na uhakika
wa kumweka mfalme juu yenu ambaye
BWANA Mungu wenu atamchagua. Ni lazima
atoke miongoni mwa ndugu zenu wenyewe.
Msimweke mgeni juu yenu ambaye si ndugu
wa Kiisraeli. 16 [q]Hata hivyo, kamwe mfalme
asijipatie hesabu kubwa ya farasi kwa ajili
yake mwenyewe, au kuwafanya watu
warudi Misri ili kupata farasi zaidi, kwa
maana BWANA amekuambia, “Hamtairudia

---

[a]**16:22** Kut 23:24; Law 26:1
[b]**17:1** Kut 12:5; Law 22:20; Kum 7:25; 15:21; Mal 1:8, 13
[c]**17:2** Kum 13:6-11
[d]**17:3** Yer 7:31; Kut 22:20; Mwa 1:16; 2:1; 37:9; Ay 31:26
[e]**17:4** Kum 22:20; 13:12-14
[f]**17:5** Law 24:14
[g]**17:6** Hes 35:30; Kum 19:15; Mt 18:16; Yos 7:25; Yn 8:17
[h]**17:6** Hes 35:30; Mt 18:16; Yn 8:17; 2Kor 13:1; 1Tim 5:19; Ebr 10:28
[i]**17:7** Yn 8:7; Law 24:14; Mdo 7:58; Kum 13:5, 9; 1Kor 15:13
[j]**17:8** Kut 21:6, 13; 2Nya 19:10; Kum 12:5; Za 122:3-5; Hag 2:11; Mal 2:7; Hes 35:11; Kum 19:17
[k]**17:9** Kum 24:8; 27:9; Kut 21:6; Mwa 25:22; Kum 19:17; Eze 44:24; Hag 2:11; Amu 4:5; 1Fal 3:16
[l]**17:11** Law 10:11; Kum 5:32; 25:1
[m]**17:12** Hes 15:30; 16:9-13; Mwa 17:14; Kum 13:11; 18:20; 19:20; 1Fal 18:40; Yer 14:14; Hos 4:4; Zek 13:3; Kum 13:5
[n]**17:13** Kum 13:11
[o]**17:14** Hes 33:53; Yos 21:43; 1Sam 8:5-9; 19:20; 10:19
[p]**17:15** 1Sam 16:3; 2Sam 5:3; Yer 30:21
[q]**17:16** Isa 2:7; 30:16; 1Sam 8:11; 1Fal 4:26; 9:19; 10:26; 2Nya 1:14; Za 20:7; Isa 31:1; Yer 42:14; 1Fal 10:28-29; Eze 17:15; Kut 13:17

njia ile tena.” 17 [a]Kamwe asioe wake wengi,
la sivyo moyo wake utapotoka. Kamwe
asijilimbikizie kiasi kikubwa cha fedha na
dhahabu.
18 [b]Atakapokuwa amekalia kiti cha ufalme
wake, ajiandikie kwenye kitabu nakala ya
sheria kwa ajili yake mwenyewe kutoka
zile sheria za makuhani ambao ni Walawi.
19 [c]Atakuwa na nakala hiyo, naye ataisoma
siku zote za maisha yake ili kwamba
ajifunze kumheshimu BWANA Mungu
wake na kufuata kwa uangalifu maneno
yote ya sheria hii na amri hizi, 20 [d]naye
asijifikirie kuwa ni bora kuliko ndugu zake
na kuipotosha sheria. Ndipo yeye na wazao
wake watatawala katika ufalme wake kwa
muda mrefu katika Israeli.

*Sadaka Kwa Makuhani Na Walawi*

18 [e]Makuhani ambao ni Walawi, yaani
kabila lote la Lawi, hawatakuwa na
mgawo wala urithi pamoja na Israeli.
Wataishi kwa sadaka zitolewazo kwa ajili
ya BWANA za kuteketezwa kwa moto, kwa
maana huo ndio urithi wao. 2 [f]Hawatakuwa
na urithi miongoni mwa ndugu zao; BWANA
ndiye urithi wao, kama alivyowaahidi.
3 [g]Hili ndilo fungu la makuhani kutoka
kwa watu watakaotoa dhabihu ya fahali
au kondoo: mguu wa mbele, mataya na
matumbo. 4 [h]Mtawapa malimbuko ya nafaka
zenu, divai mpya, mafuta na sufu ya kwanza
kutoka manyoya ya kondoo zenu, 5 [i]kwa
kuwa BWANA Mungu wenu amewachagua
pamoja na wazao wao kutoka makabila
yenu kusimama na kuhudumu katika jina
la BWANA siku zote.
6 [j]Ikiwa Mlawi atahama kutoka
mmojawapo ya miji yenu popote katika
Israeli ambapo anaishi, akaja kwa moyo
wote mahali ambapo BWANA atapachagua,
7 [k]anaweza akahudumu katika jina la
BWANA Mungu wake kama Walawi
wenzake wote wanaohudumu hapo mbele
za BWANA. 8 [l]Atashiriki sawa katika mafao
yao, hata kama amepokea fedha kutoka
mauzo ya mali ya jamaa yake.

*Matendo Ya Machukizo*

9 [m]Wakati mtakapoingia katika nchi
ambayo BWANA Mungu wenu anawapa,
msijifunze kuiga njia za machukizo za
mataifa ya huko. 10 [n]Asionekane mtu
yeyote miongoni mwenu ampitishaye
mwanawe au binti yake katika moto,
atakayefanya uaguzi, ulozi, anayetabiri
nyakati, anayejishughulisha na uchawi,
11 [o]wala arogaye kwa kupiga mafundo, wala
mwaguzi au anayeabudu mizimu, wala
awaombaye wafu. 12 [p]Mtu yeyote afanyaye
mambo haya ni chukizo kwa BWANA,
tena ni kwa sababu ya matendo haya ya
kuchukiza wayafanyayo ndiyo maana
BWANA Mungu wenu atayafukuza mataifa
hayo mbele yenu. 13 [q]Kamwe msilaumiwe
mbele za BWANA Mungu wenu.

*Nabii*

14 [r]Mataifa mtakayowafukuza husikiliza
wale wafanyao ulozi na uaguzi. Lakini
kwenu ninyi, BWANA Mungu wenu
hajawaruhusu kufanya hivyo. 15 [s]BWANA
Mungu wenu atawainulia nabii kama
mimi kutoka miongoni mwa ndugu zenu

[a]**17:17** Kut 34:16; 2Sam 5:13; 12:11; 1Fal 11:3; 2Nya 11:21; Za 31:3
[b]**17:18** 2Fal 11:12; Kum 31:9; 2Fal 22:8
[c]**17:19** Yos 8; Za 119:97
[d]**17:20** Kum 5:32
[e]**18:1** Yer 33:21; Hes 18:8, 20; 1Kor 9:13
[f]**18:2** Hes 18:20; Yos 13:14
[g]**18:3** Kut 29:27; Law 1:5; 7:28-34; Hes 18:12
[h]**18:4** Kut 22:29; Hes 18:12
[i]**18:5** Kut 28:1; 29:9; Kum 10:8; Kut 29:9
[j]**18:6** Hes 35:2-3; Kum 12:5
[k]**18:7** 1Fal 18:32; 22:16; Za 118:26
[l]**18:8** Hes 18:24; 2Nya 31:4; Neh 12:44, 47; 13:12
[m]**18:9** Kum 9:5; 12:29-31; Law 18:3; 2Fal 21:2; 2Nya 28:3; 33:2; 34:33; Ezr 6:21; 9:11; Yer 44:4
[n]**18:10** Law 18:21; 1Sam 15:23; Kut 7:11; Law 19:31; Kum 12:31
[o]**18:11** Isa 47:9; Kut 22:18; 1Sam 28:13
[p]**18:12** Law 18:24; Kum 9:4
[q]**18:13** Mwa 6:9; 17:1; Za 119:1; Mt 5:48
[r]**18:14** 2Fal 21:6
[s]**18:15** Mt 21:11; Lk 2:25-35; Yn 1:21; Mdo 3:22; 7:37; Hes 24:17; Isa 11:1; 61:1; Mt 11:3; 21:11; Lk 2:25-34; 4:16-22; 7:16; 24:19; Yn 4:19-26; 6:14; 7:40

wenyewe. Msikilizeni yeye. 16 [a]Kwa kuwa
hivi ndivyo mlivyomwomba Bwana Mungu
wenu kule Horebu siku ile ya kusanyiko,
wakati mliposema, "Na tusiisikie sauti ya
Bwana Mungu wetu, wala kuuona moto
huu mkubwa tena, ama sivyo tutakufa."
17 Bwana akaniambia: "Wanachosema
ni vyema. 18 [b]Nitawainulia nabii kama
wewe kutoka miongoni mwa ndugu
zao; nitaweka maneno yangu kinywani
mwake, naye atawaambia kila kitu
nitakachomwamuru. 19 [c]Kama mtu yeyote
hatasikiliza maneno yangu ambayo huyo
nabii atayasema kwa Jina langu, mimi
mwenyewe nitamwajibisha. 20 [d]Lakini nabii
ambaye atathubutu kusema kwa Jina langu
kitu chochote ambacho sikumwamuru
akiseme, au nabii ambaye husema kwa
jina la miungu mingine ni lazima auawe."
21 Mnaweza kuulizana wenyewe,
"Tutawezaje kujua wakati ujumbe
haukusemwa na Bwana?" 22 [e]Ikiwa kile
nabii anachotangaza kwa jina la Bwana
hakikutokea au kutimia, huo ni ujumbe
ambao Bwana hakusema. Nabii huyo
amesema kwa ujuaji. Msimwogope huyo.

*Miji Ya Makimbilio*

**(Hesabu 35:9-34; Yoshua 20:1-9)**

19 [f]Wakati Bwana Mungu wenu
atakapokuwa amewaangamiza mataifa
ambayo nchi yao anawapa ninyi, wakati
mtakapokuwa mmewafukuza na kuishi
katika miji yao na nyumba zao, 2 [g]ndipo
mtenge miji mitatu iliyopo katikati ya nchi
kwa ajili yenu, katika nchi ambayo Bwana
Mungu wenu anawapa kuimiliki. 3 Jengeni
barabara katika miji hiyo na kuigawa mara
tatu, nchi anayowapa Bwana Mungu wenu
kama urithi, ili kwamba yeyote amuuaye
mtu aweze kukimbilia humo.
4 Hii ndiyo kanuni kuhusu mtu amuuaye
mwingine na kukimbilia humo kuokoa
maisha yake, yaani, yeye amuuaye jirani
yake bila kukusudia, wala hakumchukia
kabla ya hapo. 5 Kwa mfano, mtu aweza
kwenda msituni na jirani yake kukata miti,
naye anapozungusha shoka kuangusha
mti, shoka linaweza kuchomoka kutoka
kwenye mpini na kumpiga jirani yake na
kumuua. Yule mtu anaweza kukimbilia
katika mmojawapo ya miji hii na kuokoa
maisha yake. 6 [h]Kama sivyo, mlipiza kisasi
cha damu anaweza kumfuatilia kwa hasira
kali, naye akamkamata na kumuua kama
umbali ni mrefu sana hata ingawa hastahili
kifo, kwa sababu amemuua jirani yake bila
kukusudia. 7 Hii ndiyo sababu nimewaagiza
ninyi kutenga miji mitatu ya makimbilio
kwa ajili yenu.
8 [i]Kama Bwana Mungu wenu akipanua
nchi yenu, kama alivyoahidi kwa kiapo
kwa baba zenu na kuwapa nchi yote
aliyowaahidi, 9 [j]kwa sababu mmefuata
kwa uangalifu sheria zote ninazowaamuru
leo, kumpenda Bwana Mungu wenu na
kuenenda siku zote katika njia zake,
ndipo mtenge miji mingine, mitatu zaidi.
10 [k]Fanyeni hivi ili damu isiyo na hatia
isimwagwe katika nchi yenu, ambayo
Bwana Mungu wenu anawapa kama urithi
wenu, ili kwamba msije mkawa na hatia ya
kumwaga damu.
11 [l]Lakini kama mtu anamchukia
ndugu yake, akamvizia, akamshambulia
na kumuua, kisha akakimbilia katika
mmojawapo ya miji hii, 12 wazee wa mji
wake watatuma ujumbe kwake, kumleta
kutoka mji ule na kumkabidhi mlipiza kisasi
cha damu kumuua. 13 [m]Msimwonee huruma.

---

[a]**18:16** Kut 20:19; Kum 5:23-27
[b]**18:18** Mwa 20:7; Isa 2:3; 26:8; 51:4; Mik 4:2; Kut 4:12; Yn 4:25-26; 14:24; Mdo 3:22; Yn 17:8; 4:25; 8:28; 12:49, 50
[c]**18:19** Kut 23:21; Law 19:12; 2Fal 2:24; Yos 22:23; Mdo 3:23; Ebr 12:25
[d]**18:20** Kut 23:13; Kum 13:1-5; 17:12; Yer 14:14; 2:8; Zek 13:3
[e]**18:22** Kum 13:2; 1Sam 3:20; 1Fal 22:28; Yer 28:9
[f]**19:1** Kum 6:10-11; 12:29
[g]**19:2** Yos 20:2
[h]**19:6** Hes 35:12
[i]**19:8** Kut 34:24; Mwa 15:18; Kum 11:24
[j]**19:9** Kum 6:5; Yos 20:7-8
[k]**19:10** Mit 6:17; Yer 7:6; 26:15; Kum 21:1-9; Hes 35:33
[l]**19:11** Kut 21:12; Hes 35:16; 1Yn 3:15; Mit 28:17; 29:10
[m]**19:13** Kum 7:2; 21:9; 1Fal 2:31

Lazima mwondoe katika Israeli hatia ya
umwagaji damu isiyo na hatia ili kwamba
mpate kufanikiwa.
[14] [a]Usisogeze jiwe la mpaka wa jirani yako
ambao uliwekwa na wale waliokutangulia
katika urithi upokeao katika nchi Bwana
Mungu wako anayowapa kuimiliki.

### *Mashahidi*

[15] [b]Shahidi mmoja hatoshi kumtia hatiani
mtu kwa uhalifu au kosa lolote ambalo
anaweza kuwa amelitenda. Lazima shauri
lolote lithibitishwe kwa ushuhuda wa
mashahidi wawili au watatu.
[16] [c]Kama shahidi mwenye nia ya kumdhuru
mwingine akisimama kumshtaki mtu kwa
uhalifu, [17] [d]watu wawili wanaohusika katika
mabishano lazima wasimame mbele za
Bwana na mbele ya makuhani na waamuzi
ambao wako kazini wakati huo. [18] [e]Waamuzi
lazima wafanye uchunguzi kwa makini na
shahidi akionekana kuwa ni mwongo, akitoa
ushuhuda wa uongo dhidi ya ndugu yake,
[19] [f]basi mtende kama alivyotaka kumtendea
ndugu yake. Ni lazima mwondoe uovu
miongoni mwenu. [20] [g]Watu watakaosalia
watasikia hili na kuogopa, uovu kama
huo kamwe hautatendeka tena miongoni
mwenu. [21] [h]Msionyeshe huruma, uhai kwa
uhai, jicho kwa jicho, jino kwa jino, mkono
kwa mkono, mguu kwa mguu.

### *Kwenda Vitani*

20 [i]Mtakapokwenda vitani kupigana
na adui zenu na mkaona farasi na
magari ya vita na jeshi kubwa kuliko lenu,
msiwaogope, kwa sababu Bwana Mungu
wenu aliyewatoa kutoka Misri, atakuwa
pamoja nanyi. [2] Wakati mtakapokaribia
kwenda vitani, kuhani atakuja mbele na
kuhutubia jeshi. [3] [j]Atasema: "Sikia, ee
Israeli, leo unakwenda vitani kupigana
na adui zako. Usife moyo wala usiogope,
usitishwe wala usitiwe hofu mbele yao.
[4] [k]Kwa kuwa Bwana Mungu wenu ndiye
huenda pamoja nanyi kuwapigania dhidi
ya adui zenu na kuwapatia ushindi."
[5] [l]Maafisa wataliambia jeshi: "Je,
kuna yeyote aliyejenga nyumba mpya
ambayo haijawekwa wakfu? Yeye na
arudi nyumbani, ama sivyo anaweza kufa
vitani na mtu mwingine akaiweka wakfu.
[6] [m]Je, kuna yeyote aliyepanda shamba la
mizabibu na hajaanza kulifurahia? Yeye
na arudi nyumbani, au sivyo anaweza
kufa vitani na mtu mwingine akalifurahia.
[7] [n]Je, kuna yeyote aliyeposa mwanamke na
hajamwoa? Yeye na arudi nyumbani, ama
sivyo anaweza kufa vitani na mtu mwingine
akamwoa." [8] [o]Kisha maafisa wataongeza
haya, "Je, kuna mtu anayeogopa ama kufa
moyo? Yeye na arudi nyumbani ili ndugu
zake nao wasije wakafa moyo pia." [9] Wakati
maafisa watakapomaliza kuzungumza na
jeshi, watawateua wakuu wa vikosi.
[10] [p]Wakati mtakapokwenda kushambulia
mji, wapeni watu wake masharti ya amani.
[11] [q]Wakikubali na kuwafungulia malango
yao, watu wake wote watawatumikia kwa
kufanya kazi ngumu na watawatumikia.
[12] Ikiwa watakataa kufanya mapatano ya
amani na wakiwaingiza katika vita, basi
mtauzunguka mji huo kwa vita. [13] [r]Wakati
Bwana Mungu wenu atakapouweka mji

[a]**19:14** Kum 27:17; Ay 24:2; Za 16:6; Mit 15:25; 22:28; 23:10; Isa 1:23; Hos 5:10
[b]**19:15** Kum 17:6; Mt 18:16; 26:60; 2Kor 3:1; Yn 8:17; 1Tim 5:19; Ebr 10:28
[c]**19:16** Kut 23:1; Mit 6:19; Za 27:12; 1Fal 21:13
[d]**19:17** Kut 21:6; Kum 17:6
[e]**19:18** Kut 23:7
[f]**19:19** Mit 19:5-10; 1Kor 5:13; Dan 6:24
[g]**19:20** Kum 13:11; 17:13; 13:13; 21:21
[h]**19:21** Kut 21:24; Mt 5:38
[i]**20:1** Za 20:7; Isa 31:1; Hes 14:9; Kum 3:22; 1Sam 17:45; Isa 41:10; 2Nya 32:7-8; Hes 23:21; Kum 31:6, 8; 2Nya 13:12; 32:7, 8
[j]**20:3** 1Sam 17:32; Ay 23:16; Za 22:14; Isa 7:4; 35:4; Yer 51:46
[k]**20:4** 2Nya 20:14-22; Kut 14:14; 1Nya 5:22; Neh 4:20; Amu 12:3; 15:18; Za 44:7; 144:10; Kum 1:30
[l]**20:5** Neh 12:27
[m]**20:6** Yer 31:5; Eze 28:26; Mik 1:6; 1Kor 9:7
[n]**20:7** Kum 24:5; Mit 5:18
[o]**20:8** Amu 7:3
[p]**20:10** Kum 2:26; Lk 14:31-32; 2Sam 20:18-20
[q]**20:11** 2Fal 6:22; 1Fal 9:21; 1Nya 22:2; Isa 31:7
[r]**20:13** Hes 31:7

huo mkononi mwenu, waueni kwa upanga
wanaume wote waliomo ndani yake. [14] [a]Kwa
upande wa wanawake, watoto, mifugo na
kila kitu kingine chochote ndani ya huo mji,
mnaweza kuvichukua kama nyara kwa ajili
yenu. Nanyi mnaweza kuzitumia hizo nyara
ambazo BWANA Mungu wenu amewapa
kutoka kwa adui zenu. [15] [b]Hivi ndivyo
mtakavyofanya kwa miji yote ambayo
iko mbali nanyi, ambayo haimilikiwi na
mataifa ya karibu.

[16] [c]Hata hivyo, katika miji ya mataifa
ambayo BWANA Mungu wenu anawapa
kama urithi, msiache kitu chochote hai
kinachopumua. [17] Waangamizeni kabisa
Wahiti, Waamori, Wakanaani, Waperizi,
Wahivi na Wayebusi, kama BWANA
Mungu wenu alivyowaamuru. [18] [d]La sivyo,
watawafundisha kufuata mambo yote
ya machukizo wanayofanya wakiabudu
miungu yao, nanyi mtatenda dhambi dhidi
ya BWANA Mungu wenu.

[19] Wakati mtakapouzunguka mji kwa vita
kwa muda mrefu, mkipigana dhidi yake ili
kuuteka, msiharibu miti yake kwa kuikata
kwa shoka, kwa sababu mtaweza kula
matunda yake. Hivyo msiikate. Je, miti hiyo
ya mashambani ni watu, hata muizingire?
[20] Hata hivyo, mnaweza kuikata miti
ambayo sio miti ya matunda na kuitumia
kujenga ngome, mpaka mji ulio katika vita
na ninyi utakapoanguka.

### *Upatanisho Kuhusu Mauaji*

21 [e]Kama mtu akikutwa ameuawa, naye
amelala kwenye shamba katika nchi
ambayo BWANA Mungu wenu anawapa
kuimiliki, wala haijulikani ni nani
aliyemuua, [2] wazee wenu na waamuzi
watatoka na kupima umbali kutoka maiti
alipolala mpaka kwenye miji ya jirani.
[3] [f]Kisha wazee wa ule mji ulio karibu
zaidi na yule maiti watamchukua mtamba
ambaye hajapata kufanyishwa kazi na
ambaye hajafungwa nira, [4] na kumpeleka
kwenye bonde ambalo halijapata kulimwa
au kupandwa mazao na ambapo kuna
chemchemi itiririkayo. Huko kwenye hilo
bonde, wazee watamvunja yule mtamba
shingo. [5] [g]Makuhani, hao wana wa Lawi,
watasogea mbele, kwa kuwa BWANA
Mungu wenu, amewachagua kuhudumu
na kutoa baraka katika jina la BWANA,
na kuamua mashauri yote ya mabishano
na mashambulio. [6] [hi]Ndipo wazee wote
wa mji ulio karibu zaidi na huyo maiti
watanawa mikono yao juu ya huyo
mtamba ambaye shingo yake imevunjwa
huko kwenye bonde, [7] [j]nao watatangaza:
"Mikono yetu haikumwaga damu hii,
wala macho yetu hayakuona likifanyika.
[8] [k]Ee BWANA, ukubali upatanisho kwa
watu wako Israeli, ambao umewakomboa,
wala usiwahesabie watu wako hatia ya
damu ya mtu asiyekuwa na hatia." Nayo
damu iliyomwagika itakuwa imefanyiwa
upatanisho. [9] [l]Hivyo mtakuwa mmejitakasa
wenyewe kutoka hatia ya kumwaga damu
isiyokuwa na hatia, kwa kuwa mmefanya
lile lililo sawa mbele za macho ya BWANA.

### *Kuoa Mwanamke Mateka*

[10] [m]Mkienda vitani kupigana na adui
zenu naye BWANA Mungu wenu akawatia
adui mikononi mwenu, nanyi mkachukua
mateka, [11] [n]kama ukiona miongoni
mwa mateka mwanamke mzuri wa sura
nawe wavutwa naye, waweza kumwoa

---

[a]**20:14** Yos 8:2; 22:8; Hes 31:11; 31:53
[b]**20:15** Yos 9:9
[c]**20:16** Kut 23:31-33; Hes 21:2-3; Kum 7:2; Yos 6:21; 10:1; 11:14
[d]**20:18** Kut 34:16; 10:7; 23:33; Kum 12:30-31; Yos 23:12-13; 1Kor 15:33; 2Fal 21:3, 15; Za 106:34-41; Hos 8:11
[e]**21:1** Hes 25:17; Za 9:12; Mit 28:17
[f]**21:3** Hes 19:2
[g]**21:5** Mwa 48:20; Kut 39:43; Kum 17:8-11
[h]**21:6** Mt 27:24; 1Nya 23:13
[i]**21:6** Ay 9:30; Za 19:12; Yer 2:22; Mt 27:14; Ebr 9:10
[j]**21:7** 2Sam 3:28
[k]**21:8** Hes 35:33-34; Yer 26:15; Eze 22:3; Yn 1:14
[l]**21:9** Kum 19:13
[m]**21:10** Yos 21:44; 1Fal 8:46; 1Nya 9:1; Ezr 5:12; Yer 40:1; Eze 1:1; 17:12; Dan 2:25; Mik 4:10; 2Nya 32:8
[n]**21:11** Mwa 6:2; 34:8

akawa mke wako. [12] [a]Mlete nyumbani mwako, anyoe nywele na kukata kucha zake, [13] [b]avue nguo alizokuwa amevaa alipotekwa. Baada ya kuishi nyumbani mwako na kumwombolezea baba yake na mama yake kwa mwezi mzima, ndipo utakapoweza kumwendea na kuwa mume wake naye atakuwa mke wako. [14] [c]Lakini kama hutaendelea kupendezwa naye, mwache aende popote anapotaka. Kamwe huwezi kumuuza au kumtendea kama mtumwa, kwa sababu utakuwa umemvunjia heshima.

*Haki Ya Mzaliwa Wa Kwanza*

[15] [d]Kama mwanaume ana wake wawili, naye anampenda mmoja na mwingine hampendi na wote wawili wamemzalia wana wa kiume, lakini mwana mzaliwa wa kwanza ni wa yule mke asiyempenda, [16] [e]wakati anapotoa wosia wa mali yake kwa wanawe, kamwe asitoe haki za mzaliwa wa kwanza kwa mwana wa mke ampendaye kwa upendeleo, badala ya mzaliwa hasa wa kwanza, ambaye ni mwana wa mke ambaye hampendi. [17] [f]Ni lazima amkubali mwana wa mke asiyempenda kama mzaliwa wa kwanza kwa kumpa sehemu ya vile vyote alivyo navyo maradufu. Mwana huyo ni ishara ya kwanza ya nguvu za baba yake. Haki ya mzaliwa wa kwanza ni yake yeye.

*Mwana Mwasi*

[18] [g]Kama mtu ana mwana mkaidi na mwasi ambaye hamtii baba yake na mama yake, na hasikii wazazi wanapomrudi, [19] baba yake na mama yake watamleta kwa wazee kwenye lango la mji wake. [20] Watawaambia wazee, "Huyu mwanetu ni mkaidi na mwasi. Hatutii sisi, yeye ni mpotovu na mlevi." [21] [h]Kisha wanaume wote wa mjini mwake watampiga kwa mawe mpaka afe. Ndivyo imewapasa kuondoa maovu kati yenu. Israeli yote itasikia hili na kuogopa.

*Sheria Mbalimbali*

[22] [i]Kama mtu ana hatia ya kosa linalompasa kuuawa naye akauawa, mwili wake utaangikwa mtini, [23] [j]kamwe msiuache mwili wake mtini usiku kucha. Hakikisheni mnauzika mwili wake siku ile ile, kwa sababu kila mtu anayeangikwa mtini yupo chini ya laana ya Mungu. Msiinajisi nchi ambayo Bwana Mungu wenu anawapa kama urithi wenu.

22 [k]Kama ukimwona ng'ombe au kondoo wa ndugu yako anapotea, usipuuze, bali uhakikishe unamrudisha kwa mwenyewe. [2] Ikiwa huyo ndugu haishi karibu nawe au kama hufahamu yeye ni nani, mchukue nyumbani kwako huyo mnyama umweke mpaka mwenyewe aje kumtafuta. Ndipo umrudishie. [3] Fanya vivyo hivyo ukimkuta punda wa nduguyo au joho lake au chochote alichopoteza. Usipuuze jambo hilo.

[4] [l]Kama ukimwona punda wa nduguyo au ng'ombe wake ameanguka barabarani, usipuuze jambo hilo. Msaidie asimame kwa miguu yake.

[5] [m]Haimpasi mwanamke kuvaa nguo za kiume wala mwanaume kuvaa nguo za kike, kwa maana Bwana Mungu wenu anachukia yeyote ambaye hufanya hivi.

[6] [n]Kama ukikuta kiota cha ndege kando ya barabara, iwe juu ya mti au chini, naye ndege amelala juu ya makinda au mayai, usimchukue huyo ndege pamoja na makinda

[a]**21:12** Law 14:9; Hes 8:7; 1Kor 11:5; Hes 6:9
[b]**21:13** Za 45:10
[c]**21:14** Mwa 34:2; Amu 19:24
[d]**21:15** Mwa 4:19; 29:33
[e]**21:16** 1Nya 26:10; Rum 8:29
[f]**21:17** 2Fal 2:9; Isa 40:2; 61:7; Zek 9:12; Mwa 49:3; 25:31; Lk 15:12; 1Nya 5:1
[g]**21:18** Za 78:8; Yer 5:23; Sef 3:1; Mit 30:17; Mwa 31:35; Mit 1:8; Isa 30:1; Efe 6:1-3; Kut 20:12; 21:15, 17; Law 19:3; 21:9
[h]**21:21** Law 20:9; Kum 19:19; 1Kor 5:13; Kum 13:11; 1Sam 26:16
[i]**21:22** Kum 22:26; Mt 26:66; Mk 14:64; Mdo 23:29
[j]**21:23** Yos 8:29; 10:27; Yn 19:31; Eze 39:12; Ezr 6:11; Es 2:23; 7:9; 8:7; 9:13, 25; Isa 50:11; Gal 3:13; Law 18:25
[k]**22:1** Kut 23:4-5; Mit 27:10; Zek 7:9
[l]**22:4** Kut 23:5; 1Kor 9:9; Rum 12:10; 2Pet 1:7; 1Yn 3:15; 4:21; Zek 7:9
[m]**22:5** 1Kor 14:40
[n]**22:6** Law 22:28; Neh 9:6; Za 36:6; 145:9; Mt 10:29; Lk 12:6

yake. 7 [a]Waweza kuchukua makinda, lakini
uwe na hakika ya kumwacha huyo ndege, ili
upate kufanikiwa na uweze kuishi maisha
marefu.
8 [b]Wakati unapojenga nyumba mpya,
fanya ukuta wa kuzuia kandokando ya dari
ili usijiletee hatia ya kumwaga damu juu
ya nyumba yako ikiwa yeyote ataanguka
kutoka humo.
9 [c]Usipande aina mbili za mbegu katika
shamba lako la mizabibu; ikiwa utafanya
hivyo, si mazao utakayopanda tu yatakuwa
najisi, bali nayo matunda ya shamba la
mizabibu pia.
10 [d]Usilime kwa maksai aliyefungwa nira
pamoja na punda.
11 [e]Usivae nguo za sufu na kitani
zilizofumwa pamoja.
12 [f]Fanya vishada kwenye pembe nne za
joho unalovaa.

*Kukiuka Taratibu Za Ndoa*

13 [g]Ikiwa mtu atamwoa mke na, baada ya
kufanya naye tendo la ndoa, akamchukia,
14 akimsingizia na kumwita jina baya,
akisema, "Nilimwoa mwanamke huyu,
lakini nilipomkaribia sikupata uthibitisho
wa ubikira wake" 15 [h]ndipo baba na mama
wa msichana wataleta uthibitisho kwamba
alikuwa bikira kwa wazee wa mji kwenye
lango. 16 Baba wa msichana atawaambia
wazee, "Nilimwoza binti yangu kwa huyu
mwanaume, lakini hampendi. 17 Sasa
amemsingizia na kusema, 'Sikumkuta
huyu binti akiwa bikira.' Lakini hapa
kuna uthibitisho wa ubikira wa binti
yangu." Kisha wazazi wake wataonyesha
nguo zake kwa wazee wa mji, 18 [i]nao
wazee watamchukua huyo mwanaume
na kumwadhibu. 19 Watamtoza shekeli
mia moja[j] za fedha na kupewa wazazi wa
msichana, kwa sababu mwanaume huyu
amempa bikira wa Kiisraeli jina baya.
Ataendelea kuwa mke wake; kamwe hawezi
kumpa talaka siku zote za maisha yake.
20 [k]Hata hivyo, kama shtaka ni la kweli na
hakuna uthibitisho juu ya ubikira wa huyo
msichana ulioweza kupatikana, 21 [l]huyo
msichana ataletwa kwenye mlango wa
nyumba ya baba yake, na hapo watu wa
mji wake watampiga kwa mawe hadi afe.
Amefanya kitu cha aibu katika Israeli kwa
kufanya ukahaba akiwa nyumbani kwa
babaye. Lazima mwondoe uovu katikati
yenu.
22 [m]Ikiwa mwanaume atakutwa akizini
na mke wa mtu mwingine, wote wawili,
mwanaume na mwanamke aliyezini naye,
lazima wauawe. Lazima mwondoe uovu
katika Israeli.
23 [n]Ikiwa mwanaume atakutana na bikira
mjini ambaye ameposwa na mtu akazini
naye, 24 [o]utawachukua wote wawili kwenye
lango la mji na kuwapiga kwa mawe mpaka
wafe; yule msichana kwa kuwa alikuwa
mjini na hakupiga kelele kuomba msaada,
na yule mwanaume kwa sababu amemtenda
jeuri mke wa mtu mwingine. Lazima
mwondoe uovu katikati yenu.
25 Lakini ikiwa itatokea mwanaume
akakutana na msichana aliyeposwa huko
mashambani, akambaka, mwanaume
aliyefanya hivi peke yake ndiye
atakayeuawa. 26 Usimtendee msichana
yule jambo lolote; hajafanya dhambi
inayostahili kifo. Shauri hili ni kama lile
la yeyote ambaye anamshambulia na
kumuua kwa makusudi jirani yake, 27 [p]kwa
maana mwanaume huyo alimkuta msichana
huko mashambani, na ingawa msichana

---

[a]**22:7** Law 22:28; Kum 5:29; 4:20
[b]**22:8** Yos 2:8; 1Sam 11:2
[c]**22:9** Law 19:9; Mt 6:24; 9:16; 2Kor 6:14-16
[d]**22:10** 2Kor 6:14-16
[e]**22:11** Law 19:9; 19:19
[f]**22:12** Hes 15:37-41; Mt 23:5
[g]**22:13** Kum 24:1; Mwa 29:21; Amu 15:1; Efe 5:28-29
[h]**22:15** Mwa 23:10
[i]**22:18** Kut 18:21; Kum 1:9-18; Rum 13:3
[j]19 Shekeli 100 za fedha ni sawa na kilo moja.
[k]**22:20** Kum 17:4
[l]**22:21** Mwa 34:7; 38:24; Law 19:29; Kum 23:17-18; 1Kor 5:13; 2Sam 13:12, 13
[m]**22:22** 2Sam 11:4; Mwa 38:24; Kut 21:12; Mt 5:27-28; Yn 8:5; 1Kor 6:9; Ebr 13:4; Law 20:10; Mit 6:22; Mal 3:5; Yn 8:5
[n]**22:23** Mt 1:18, 19
[o]**22:24** 1Kor 5:13; Kum 21:14; Mt 1:20, 24
[p]**22:27** Mwa 39:14

aliyeposwa alipiga kelele, hapakuwa na mtu
wa kumwokoa.
28 [a]Ikiwa itatokea mwanaume akutane na
bikira ambaye hajaposwa na kumbaka nao
wakakutwa, 29 mwanaume atamlipa baba
wa msichana shekeli hamsini[b] za fedha. Ni
lazima amwoe huyo msichana, kwa maana
amemfanyia jeuri. Kamwe hawezi kumpa
talaka siku zote za maisha yake.
30 [c]Mwanaume asimwoe mke wa baba
yake; kamwe asidhalilishe kitanda cha
baba yake.

*Kutengwa Na Mkutano*

23 [d]Asiingie mtu yeyote aliyehasiwa kwa
kupondwa makende au kwa kukatwa
uume wake katika kusanyiko la Bwana.
2 Mtu yeyote ambaye amezaliwa kwenye
ndoa isiyo halali au wazao wake wasiingie
kwenye kusanyiko la Bwana, hata mpaka
kizazi cha kumi.
3 [e]Hapatakuwa na Mwamoni au Mmoabu
au yeyote wa wazao wao atakayeruhusiwa
kuingia katika kusanyiko la Bwana, hata
mpaka kizazi cha kumi. 4 [f]Kwa kuwa
hawakuja kuwalaki wakiwa na mkate na
maji mlipokuwa njiani mlipotoka Misri,
tena walimwajiri Balaamu mwana wa Beori
kutoka Pethori iliyoko Aramu-Naharaimu[g]
ili kuwalaani ninyi. 5 [h]Hata hivyo, Bwana
Mungu wenu hakumsikiliza Balaamu bali
aligeuza laana kuwa baraka kwenu kwa
sababu Bwana Mungu wenu anawapenda.
6 [i]Msitafute mapatano ya urafiki nao maisha
yenu yote.
7 [j]Usimchukie Mwedomu, kwa kuwa yeye
ni ndugu yako. Usimchukie Mmisri, kwa
sababu uliishi kama mgeni katika nchi yake.
8 Kizazi cha tatu cha watoto watakaozaliwa
nao wanaweza kuingia katika kusanyiko
la Bwana.

*Unajisi Katika Kambi*

9 Unapokuwa umepiga kambi dhidi ya
adui zako, jitenge na kitu chochote kisicho
safi. 10 [k]Ikiwa mtu amechafuka kwa sababu
ya kutokwa na shahawa usiku, inampasa
atoke nje ya kambi na kukaa huko. 11 [l]Lakini
jioni ikikaribia ataoga, na baada ya jua
kuzama ataingia tena kambini.
12 Tengeni mahali nje ya kambi ambapo
mnaweza kwenda kujisaidia. 13 Kama
sehemu ya vifaa vyenu kuweni na kitu cha
kulimia, nanyi mnapojisaidia, chimba shimo
na kisha funika kile kikutokacho. 14 [m]Kwa
kuwa Bwana Mungu wenu hutembea katika
kambi yenu ili kuwalinda na kuwaweka
adui zenu mikononi mwenu. Kambi yenu ni
lazima iwe takatifu, ili asione kitu chochote
miongoni mwenu kilicho kichafu akageuka
na kuwaacha.

*Sheria Mbalimbali*

15 [n]Ikiwa mtumwa amekimbilia kwako,
usimrudishe kwa bwana wake. 16 [o]Mwache
aishi miongoni mwenu mahali popote
anapopapenda na katika mji wowote
anaochagua. Usimwonee.

---

[a]**22:28** Kut 22:16, 17
[b]29 Shekeli 50 za fedha ni sawa na gramu 600.
[c]**22:30** Mwa 29:29; Law 18:8; 20:9; Kum 27:20
[d]**23:1** Law 21:20
[e]**23:3** Mwa 19:38; Neh 13:2; Rut 4:5; Neh 4:3-7
[f]**23:4** Kum 2:28; Hes 23:7; 2Pet 2:15; Mwa 24:10; 14:18; Kum 2:29; 1Sam 25:11; 1Fal 18:4; Isa 63:9
[g]4 Yaani Mesopotamia ya Kaskazini-Magharibi.
[h]**23:5** Hes 24:10; Yos 24:10; Mit 26:2; Kum 4:37
[i]**23:6** Hes 24:17; Isa 15:1; 25:10; Yer 25:21; 27:3; 48:1; Eze 25:8; Sef 2:9; Ezr 9:12; Mt 5:43
[j]**23:7** Mwa 25:30; 25:26; Law 19:34; Kut 23:9; Oba 1:11-12; Law 15:1-33; Kum 10:19; Law 19:34
[k]**23:10** Law 15:16
[l]**23:11** Law 15:16; 1Sam 21:5
[m]**23:14** Mwa 3:8; Kut 3:4-5; Law 26:12; Yer 32:40; 2Kor 6:16
[n]**23:15** 2Sam 22:3; Za 2:12; 71:1; 1Sam 30:15
[o]**23:16** Kut 22:21; 23:6; Mt 22:22; Yer 7:6; Zek 7:10; Yak 2:6

17 [a]Asiwepo Mwisraeli mwanamke
kahaba au mwanaume hanithi wa mahali
pa kuabudia miungu. 18 [b]Kamwe usilete
mapato ya ukahaba ikiwa ni ya mwanamke
au ni ya mwanaume katika nyumba ya
Bwana Mungu wako kwa ajili ya nadhiri
yoyote, kwa sababu Bwana Mungu wako
anachukizwa na yote mawili.
19 [c]Usimtoze ndugu yako riba, iwe ni
fedha ama chakula ama kitu kingine
chochote ambacho waweza kupata riba
juu yake. 20 [d]Unaweza kumtoza mgeni riba,
lakini siyo nduguyo Mwisraeli, ili kwamba
Bwana Mungu wako akubariki katika
kila kitu unachoweka mkono katika nchi
unayoingia kuimiliki.
21 [e]Ukiweka nadhiri kwa Bwana Mungu
wako, usichelewe kuitimiza, kwa kuwa
Bwana Mungu wako atakudai, nawe
utakuwa na hatia ya dhambi. 22 [f]Lakini
ukijizuia kuweka nadhiri, hutakuwa na
hatia. 23 [g]Chochote kitakachotamkwa
kwa midomo yako ni lazima uhakikishe
umekifanya, kwa sababu uliweka nadhiri
yako kwa hiari mbele za Bwana Mungu
wako kwa kinywa chako mwenyewe.
24 [h]Kama ukiingia katika shamba la
mizabibu la jirani yako, unaweza kula
zabibu kadiri utakavyo, lakini usiweke
chochote kwenye kikapu chako. 25 [i]Kama
ukiingia katika shamba la nafaka la jirani
yako, unaweza kukwanyua kwa mikono
yako, lakini usikate kwa mundu nafaka
iliyosimama.

*Sheria Kuhusu Ndoa Na Talaka*

24 [j]Ikiwa mtu atamwoa mke na
akamchukia kwa sababu ya kukosa
adabu, naye akamwandikia hati ya talaka,
akampa na kumfukuza kutoka nyumbani
kwake, 2 ikiwa baada ya kuondoka
nyumbani kwake atakuwa mke wa mtu
mwingine, 3 ikiwa mume wake wa pili
atachukizwa naye akamwandikia hati
ya talaka, akampa na kumfukuza kutoka
nyumbani kwake, au kama akifa, 4 [k]basi
yule mume wake wa kwanza, ambaye
alimpa talaka, haruhusiwi kumwoa tena
baada ya mwanamke huyo kuwa najisi.
Hayo yatakuwa machukizo machoni pa
Bwana. Usilete dhambi juu ya nchi ambayo
Bwana Mungu wako anakupa kama urithi.
5 [l]Kama mtu ameoa karibuni, kamwe
asipelekwe vitani au kupewa wajibu
mwingine wowote. Kwa mwaka mmoja
atakuwa huru kubaki nyumbani ili
amfurahishe mke aliyemwoa.
6 [m]Usitoe jozi ya mawe ya kusagia, hata
ikiwa lile la juu, kuweka rehani kwa ajili
ya deni, kwa sababu itakuwa ni kuweka
uhai wa mtu kama dhamana.
7 [no]Kama mtu akikamatwa akiiba yeyote
miongoni mwa ndugu zake wa Waisraeli
na kumtenda kama mtumwa au akimuuza,
mwizi huyo ni lazima auawe. Nawe
utaondoa uovu kutoka miongoni mwenu.
8 [p]Pakitokea magonjwa ya ngozi ya
kuambukiza, mwe waangalifu sana kufanya
sawasawa na maagizo ya makuhani, ambao
ni Walawi. Ni lazima mfuate kwa uangalifu
yale niliyowaamuru. 9 [q]Kumbukeni kile
Bwana Mungu wenu alichomfanyia
Miriamu njiani baada ya ninyi kutoka Misri.
10 [r]Unapomkopesha jirani yako chochote,

[a]**23:17** 1Fal 14:24; 15:12; 22:46; 2Fal 23:7; Ay 36:14; Mwa 38:21; Law 19:29; Mit 2:16; Mwa 19:5
[b]**23:18** Mwa 19:5; Law 20:13; Ufu 22:15
[c]**23:19** Law 25:35-37; Neh 5:2-7; Kut 22:25; Za 15:5; Lk 6:34
[d]**23:20** Hes 6:21; Amu 11:35; Za 15:4; Hes 30:1-2; Ay 22:27; Za 61:8; 65:1; 76:11; Mhu 5:4-5; Isa 19:21; Mt 5:33; Mdo 5:3; Kum 25:10; 28:12; Law 19:34
[e]**23:21** Ay 22:27; Za 61:8; Mhu 5:4-5
[f]**23:22** Mdo 5:4
[g]**23:23** Za 66:13
[h]**23:24** Mt 12:1; Lk 12:15; 1Kor 6:10; Kol 3:5
[i]**23:25** Mt 12:1; Mk 2:23; Lk 6:1
[j]**24:1** Kum 22:13; 2Fal 17:6; Isa 50:1; Yer 3:8; Mt 1:19; 5:31; 19:7-9; Mk 10:4-5; Mal 2:16
[k]**24:4** Yer 3:1
[l]**24:5** Kum 20:7; Mit 5:18
[m]**24:6** Kut 22:22; Isa 47:2
[n]**24:7** Yer 11:2; Ebr 9:15; 10:15-17; Mwa 17:9; Kut 3:1; Kum 4:23
[o]**24:7** Kut 21:16; 1Kor 5:13
[p]**24:8** Law 13:1-46; Kum 17:9; Law 14:2; Mt 8:4; Lk 5:14; 7:14
[q]**24:9** Hes 12:10; Lk 17:32; 1Kor 10:6
[r]**24:10** Kut 22:25-27

usiingie nyumbani kwake kutwaa kile
anachokitoa kama rehani. 11 Ukae nje
na umwache huyo mtu uliyemkopesha
akuletee hiyo rehani. 12 [a]Ikiwa mtu huyo
ni maskini, usiende kulala ukiwa na hiyo
rehani yake katika milki yako. 13 [b]Rudisha
vazi lake kabla ya machweo ya jua ili
apate kulilalia. Kisha atakushukuru na
kitaonekana kama kitendo cha haki mbele
za BWANA Mungu wako.

14 [c]Usimwonee mtu maskini na mhitaji
ambaye umemwajiri, akiwa ni nduguyo
Mwisraeli au mgeni anayeishi katika
mojawapo ya miji yenu. 15 [d]Mlipe ujira wake
kila siku kabla ya jua kutua, kwa sababu
yeye ni maskini na anautegemea ujira huo.
La sivyo, anaweza kumlilia BWANA dhidi
yako, nawe ukapata hatia ya dhambi.

16 [e]Baba wasiuawe kwa ajili ya watoto
wao, wala watoto wasiuawe kwa ajili ya
baba zao; kila mmoja atakufa kwa ajili ya
dhambi yake mwenyewe.

17 [f]Usipotoshe hukumu ya mgeni au
yatima, au kuchukua vazi la mjane kama
rehani. 18 Kumbukeni kwamba mlikuwa
watumwa huko Misri, naye BWANA Mungu
wenu akawakomboa kutoka huko. Hii ndiyo
sababu ninawaamuru kutenda hili.

19 [g]Unapovuna shamba lako na ukasahau
mganda, usirudi kuuchukua. Acha kwa ajili
ya mgeni, yatima na mjane, ili BWANA
Mungu wako aweze kukubariki wewe katika
kazi zote za mikono yako. 20 [h]Unapovuna
zeituni kutoka miti yako, usirudie matawi
mara ya pili. Acha kilichobaki kwa ajili ya
mgeni, yatima na mjane. 21 Unapochuma
zabibu katika shamba lako la mizabibu
usirudie tena. Acha zinazobaki kwa ajili
ya mgeni, yatima na mjane. 22 Kumbuka
kwamba mlikuwa watumwa katika nchi ya
Misri. Ndiyo sababu ninawaamuru kufanya
hili.

25 [i]Watu wanapokuwa na ugomvi,
wapeleke mahakamani na waamuzi
wataamua shauri hilo; watawaachia wasio
na kosa na kuwahukumu wenye hatia.
2 [j]Kama mtu mwenye hatia anastahili
kuchapwa, mwamuzi atamwamuru alale
chini ili achapwe mbele yake idadi ya
viboko kulingana na kosa lake, 3 [k]lakini
kamwe asichapwe zaidi ya viboko arobaini.
Ikiwa atachapwa zaidi ya viboko arobaini,
nduguyo atadhalilika machoni pako.

4 [l]Usimfunge maksai kinywa anapopura
nafaka.

5 [m]Ikiwa ndugu wanaishi pamoja na
mmoja wao akafa bila kuacha mwana,
kamwe mjane wake asiolewe nje ya jamaa
hiyo. Ndugu wa mumewe atamchukua,
amwoe na kutimiza wajibu wa shemeji
kwake. 6 [n]Mwana wa kwanza atakayemzaa
atapewa jina la ndugu aliyekufa ili jina lake
lisifutike katika Israeli.

7 [o]Hata hivyo, ikiwa ndugu huyo wa
mume hataki kuoa huyo mke wa nduguye,
mjane atawaendea wazee kwenye lango la
mji na kusema, “Ndugu wa mume wangu
anakataa kuendeleza jina la nduguye
katika Israeli. Hataki kutimiza wajibu
wa shemeji kwangu.” 8 Ndipo wazee wa
mji wake watamwita na kuzungumza

---

[a]**24:12** Kut 22:26
[b]**24:13** Kut 22:26-27; Kum 6:25; Za 106:31; Dan 4:27; Ay 24:7, 8; 31:16-20; Eze 18:7, 12, 16; 33:15; Amo 2:8; Ay 29:11; 2Kor 9:13; 2Tim 1:18
[c]**24:14** Law 19:13; 25:35-43; Kum 15:12-18; Ay 24:4; Mit 14:31; 19:17; 1Tim 5:18; Amo 4:1; Mal 3:5
[d]**24:15** Law 25:35; 19:13; Mt 20:8; Kut 22:23; Ay 12:19; Yak 5:4; Yer 22:13
[e]**24:16** Hes 26:11; Yer 31:29-30; Eze 18:20; 2Fal 14:6
[f]**24:17** Kut 22:22; Ay 6:27; 24:9; 29:12; Za 10:17-18; 82:3; Mit 23:10; Eze 22:7; Kut 22:21; 23:2; Kum 10:18
[g]**24:19** Law 19:9; Kum 10:19; 27:19; Eze 47:22; Zek 7:10; Mal 3:5; Kum 14:29; Law 23:22; Mit 19:17; 28:27; Mhu 11:1
[h]**24:20** Law 19:10
[i]**25:1** Kut 21:6; Kum 17:8-13; 19:17; Mdo 23:3; 1Fal 8:32; Kut 23:7; Kum 1:16-17
[j]**25:2** Mit 10:13; 19:29; Lk 12:48-49
[k]**25:3** Mt 27:26; Yn 19:1; 2Kor 11:24; Ay 18:3; Yer 20:2
[l]**25:4** Hes 22:29; 1Kor 9:9; 1Tim 5:18
[m]**25:5** Rut 4:10-13; Mt 22:24; Mk 12:19; Lk 20:28
[n]**25:6** Mwa 38:9; Rut 4:5, 10
[o]**25:7** Rut 1:15; 4:2-6; Mwa 23:10

naye. Kama atashikilia kukataa akisema,
“Sitaki kumwoa,” 9 [a]mjane wa nduguye
atamwendea mbele ya wazee, atamvua
kiatu kimoja na kumtemea mate usoni, na
kusema, “Hivi ndivyo ambavyo hufanywa
kwa mtu ambaye atakataa kuendeleza
jamaa ya ndugu yake.” 10 [b]Jamaa ya mtu
huyo itafahamika katika Israeli kama Jamaa
ya Aliyevuliwa Kiatu.

11 Ikiwa watu wawili wanapigana na
mke wa mmoja wao akaja kumwokoa
mumewe na yule anayemshambulia, naye
mke huyo akifika na kumkamata sehemu za
siri, 12 [c]huyo mwanamke utamkata mkono
wake. Usimhurumie.

13 [d]Usiwe na mawe ya kupimia ya aina
mbili katika mkoba wako, moja zito na
jingine jepesi. 14 [e]Usiwe na vipimo viwili
tofauti katika nyumba yako, kimoja
kikubwa, kingine kidogo. 15 [f]Ni lazima uwe
na uzito na vipimo sahihi na vya haki, ili
upate kuishi maisha marefu katika nchi
anayokupa Bwana Mungu wako. 16 [g]Kwa
maana Bwana Mungu wako humchukia
yeyote ambaye hufanya mambo kama haya,
yeyote anayetenda kwa udanganyifu.

17 [h]Kumbuka kile Waamaleki
walichowatendea mlipokuwa njiani
mkitoka Misri. 18 [i]Wakati mlipokuwa
mmechoka na kuishiwa nguvu kwa safari
yenu, wakawapiga wale wote waliokuja
nyuma. Waamaleki hawakumwogopa
Mungu. 19 [j]Bwana Mungu wako
atakapokupa pumziko mbali na adui zako
wote wanaokuzunguka katika nchi akupayo
kuimiliki kuwa urithi, utafutilia mbali
kumbukumbu lote la Waamaleki chini ya
mbingu. Usisahau!

*Malimbuko Na Zaka*

26 Mtakapokuwa mmeingia nchi ile
ambayo Bwana Mungu wenu anawapa
kama urithi na mtakapokuwa mmeimiliki
na kukaa ndani yake, 2 [k]chukueni baadhi
ya mavuno ya kwanza ya yale yote
mtakayozalisha kutoka udongo wa nchi
ambayo Bwana Mungu wenu anawapa na
mweke kwenye kapu. Kisha uende mahali
ambapo Bwana Mungu wako atapachagua
kuwa makao kwa ajili ya Jina lake 3 na
umwambie kuhani atakayekuwepo kwa
wakati huo, “Ninatangaza leo kwa Bwana
Mungu wako kwamba nimekuja katika
nchi ambayo Bwana aliwaapia baba zetu
kwamba atatupa.” 4 Kuhani atapokea lile
kapu mikononi mwako na kuliweka chini
mbele ya madhabahu ya Bwana Mungu
wako. 5 [l]Kisha utatangaza mbele za Bwana
Mungu wako: “Baba yangu alikuwa
Mwaramu aliyekuwa anatangatanga,
akaenda Misri pamoja na watu wachache,
akaishi huko hadi akawa taifa kubwa, lenye
nguvu na watu wengi. 6 [m]Lakini Wamisri
walituonea na kututaabisha, wakitufanyisha
kazi ngumu. 7 [n]Kisha tulimlilia Bwana,
Mungu wa baba zetu, naye Bwana akasikia
sauti yetu na akaona huzuni yetu, taabu
yetu na mateso yetu. 8 [o]Kwa hiyo Bwana
akatutoa nchi ya Misri kwa mkono wenye
nguvu na ulionyooshwa, pamoja na utisho
mkuu, ishara za miujiza na maajabu.
9 [p]Akatuleta mahali hapa akatupa nchi hii,
nchi inayotiririka maziwa na asali; 10 [q]nami
sasa ninaleta malimbuko ya ardhi ambayo
wewe, Ee Bwana, umenipa.” Weka kapu

[a]**25:9** Yos 24:22; Rut 4:7-11; Hes 12:14; Ay 17:6; 30:10; Isa 50:6
[b]**25:10** Mit 6:33; 1Tim 3:7
[c]**25:12** Kum 7:2; 19:13
[d]**25:13** Mit 11:1; 20:23; Eze 45:10; Mik 6:11; Amo 8:5
[e]**25:14** Law 7:20; Hos 9:4
[f]**25:15** Kut 20:12
[g]**25:16** Mit 11:1; 20:23; Amo 8:9-11; Ufu 21:27; 1Tim 4:6; 1Kor 8:9-11
[h]**25:17** Mwa 36:12; Kut 17:8
[i]**25:18** Za 36:1; Rum 3:18; Mit 16:6
[j]**25:19** Kut 33:14; Ebr 3:18-19; Es 9:16; Mwa 36:12; 1Sam 15:2-3
[k]**26:2** Kut 22:29; 20:24; Kum 12:5; Hes 18:12; Mit 3:9; Rum 6:23; Yak 1:18
[l]**26:5** Mwa 26:13; 25:20; 34:30; 43:14; 12:2; Hes 12:12; Kum 10:22
[m]**26:6** Hes 20:15; Kut 1:13
[n]**26:7** Mwa 21:17; Kut 3:9; 2Fal 13:4; 14:26; Mwa 16:11; Za 42:9; 44:24; 72:14
[o]**26:8** Hes 20:16; Kut 3:20; Kum 4:34; 34:11-12
[p]**26:9** Kut 3:8
[q]**26:10** Kum 8:18

mbele za Bwana Mungu wako na usujudu
mbele zake. 11 [ab]Kisha wewe pamoja na
Walawi na wageni wote walioko miongoni
mwenu mtafurahi katika vitu vyote vizuri
ambavyo Bwana Mungu wenu amewapa
pamoja na wa nyumbani mwenu.
12 [c]Wakati utakapokuwa umeshatoa
zaka zote za mazao yako katika mwaka
wa tatu, ambao ni mwaka wa zaka,
utampa Mlawi, mgeni, yatima na mjane,
ili waweze kula katika miji yenu na
kushiba. 13 [d]Kisha umwambie Bwana
Mungu wako: "Nimeondoa katika nyumba
yangu ile sehemu iliyowekwa wakfu na
nimempa Mlawi, mgeni, yatima na mjane,
kulingana na yote uliyoamuru. Sijazihalifu
amri zako wala kusahau hata mojawapo.
14 [e]Sijala sehemu iliyowekwa wakfu wakati
nilipokuwa nikiomboleza, wala sijaondoa
mojawapo wakati nilipokuwa najisi, wala
sijatoa sehemu yake yoyote kwa wafu.
Nimemtii Bwana Mungu wangu; nimefanya
kila kitu ulichoniamuru. 15 [f]Angalia chini
kutoka mbinguni, maskani yako matakatifu,
uwabariki watu wako Israeli pamoja na
nchi uliyotupa kama ulivyoahidi kwa kiapo
kwa baba zetu, nchi inayotiririka maziwa
na asali."

### *Fuata Maagizo Ya Bwana*

16 [g]Bwana Mungu wako anakuagiza leo
kufuata amri hizi na sheria; zishike kwa
bidii kwa moyo wako wote na kwa roho
yako yote. 17 [h]Umetangaza leo kwamba
Bwana ndiye Mungu wako na kwamba
utafuata njia zake, kwamba utayashika
maagizo yake, amri zake na sheria zake
nawe utamtii. 18 [i]Naye Bwana ametangaza
leo kwamba ninyi ni taifa lake, hazina yake
ya thamani kama alivyoahidi, ili kwamba
mpate kuyashika maagizo yake yote.
19 [j]Ametangaza kwamba atawaweka juu
kuliko mataifa mengine aliyoyafanya katika
sifa, kuwa fahari na heshima, na kwamba
mtakuwa taifa takatifu kwa Bwana Mungu
wenu, kama alivyoahidi.

### *Madhabahu Katika Mlima Ebali*

27 [k]Mose na wazee wa Israeli wakawaagiza
watu: "Yashikeni maagizo haya yote
ninayowaagiza leo. 2 [l]Mtakapokuwa
mmevuka Mto Yordani na kuingia katika
nchi awapayo Bwana Mungu wenu,
msimamishe mawe makubwa na mkayatie
lipu. 3 [m]Andikeni juu yake maneno yote ya
sheria hii wakati mtakapokuwa mmevuka na
kuingia katika nchi awapayo Bwana Mungu
wenu, nchi itiririkayo maziwa na asali,
kama vile Bwana, Mungu wa baba zenu,
alivyowaahidi. 4 [n]Mtakapokuwa mmevuka
Yordani, simamisheni mawe haya juu ya
Mlima Ebali, kama ninavyowaagiza leo,
mkayatie lipu. 5 [o]Huko mjengeeni Bwana
Mungu wenu madhabahu, madhabahu ya
mawe. Msitumie kifaa chochote cha chuma
juu yake. 6 Jengeni madhabahu ya Bwana
Mungu wenu kwa mawe ya shambani, na
mtoe sadaka za kuteketezwa juu yake kwa
Bwana Mungu wenu. 7 [p]Toeni sadaka za
amani juu yake, mkizila na kufurahia
mbele za Bwana Mungu wenu. 8 [q]Nanyi
mtaandika maneno yote ya sheria hii kwa
wazi sana juu ya mawe haya ambayo
mmesimamisha."

---

[a]**26:11** Mit 10:22
[b]**26:11** Kum 12:7, 12, 18; Mhu 5:18-20; Isa 65:14; Mdo 2:46, 47; Flp 4:4; 1Tim 6:17; Za 63:3, 5
[c]**26:12** Mwa 14:20; Hes 18:24; Kum 14:28-29; Ebr 7:5-9; Law 27:30
[d]**26:13** Za 119:141, 153, 176
[e]**26:14** Law 7:20; 21:1, 11; Hos 9:4
[f]**26:15** Za 68:5; 80:14; 102:19; Isa 63:12; Zek 2:13; Kut 39:43; 2Nya 6:26-27; Mdo 7:49
[g]**26:16** Kum 4:29
[h]**26:17** Kut 19:8; Za 48:14
[i]**26:18** Kut 6:7; Kum 7:6
[j]**26:19** Isa 62:7; Sef 3:20; Kum 4:7-8; 28:1, 13, 44; 1Nya 14:2; Za 148:14; Isa 40:11; Kum 7:4; Kut 19:6; 1Pet 2:9
[k]**27:1** Za 78:7
[l]**27:2** Yos 4:1; Kut 24:4; Yos 24:26; 1Sam 7:12; Yos 8:31
[m]**27:3** Kut 3:8; Kum 26:9
[n]**27:4** Kum 11:29; Yos 8:30
[o]**27:5** Kut 20:24-25; Yos 8:31
[p]**27:7** Kut 32:6; Kum 16:11; Yos 8:31
[q]**27:8** Isa 8:1; 30:8; Hab 2:2; Yos 8:32

*Laana Kutoka Mlima Ebali*

9 [a]Kisha Mose na makuhani, ambao ni Walawi, wakawaambia Israeli wote, "Nyamaza ee Israeli, sikiliza! Sasa umekuwa taifa la BWANA Mungu wako. 10 Mtii BWANA Mungu wako, na kufuata amri zake na maagizo ninayokupa leo."

11 Siku ile ile Mose akawaagiza watu:

12 [b]Mtakapovuka Mto Yordani, makabila haya yatasimama juu ya Mlima Gerizimu kubariki watu: Simeoni, Lawi, Yuda,
Isakari, Yosefu na Benyamini. 13 [c]Makabila
haya yatasimama juu ya Mlima Ebali kwa kutamka laana: Reubeni, Gadi, Asheri, Zabuloni, Dani na Naftali.

14 [d]Nao Walawi watawasomea watu wote wa Israeli kwa sauti kubwa:

15 [e]"Alaaniwe mtu afanyaye sanamu ya kuchonga au mwenye kusubu sanamu, kitu ambacho ni chukizo kwa BWANA, kazi ya mikono ya fundi stadi, na kuisimamisha kwa siri."

Kisha watu wote watasema, "Amen!"

16 [f]"Alaaniwe mtu amdharauye baba yake na mama yake."

Kisha watu wote watasema, "Amen!"

17 [g]"Alaaniwe mtu asogezaye jiwe la mpaka wa jirani yake."

Kisha watu wote watasema, "Amen!"

18 [h]"Alaaniwe mtu ampotoshaye kipofu njiani."

Kisha watu wote watasema, "Amen!"

19 [i]"Alaaniwe mtu apotoshaye haki ya mgeni, yatima au mjane."

Kisha watu wote watasema, "Amen!"

20 [j]"Alaaniwe mtu akutanaye kimwili na mke wa baba yake, kwa maana anadharau malazi ya baba yake."

Kisha watu wote watasema, "Amen!"

21 [k]"Alaaniwe mtu akutanaye kimwili na mnyama yeyote."

Kisha watu wote watasema, "Amen!"

22 [l]"Alaaniwe mtu akutanaye kimwili na dada yake, binti wa baba yake au binti wa mama yake."

Kisha watu wote watasema, "Amen!"

23 [m]"Alaaniwe mtu akutanaye kimwili na mama mkwe wake."

Kisha watu wote watasema, "Amen!"

24 [n]"Alaaniwe mtu amuuaye jirani yake kwa siri."

Kisha watu wote watasema, "Amen!"

25 [o]"Alaaniwe mtu apokeaye rushwa ili kumuua mtu asiye na hatia."

Kisha watu wote watasema, "Amen!"

26 [p]"Alaaniwe mtu yule ambaye hatashikilia maneno ya sheria hii kwa kuyatekeleza."

Kisha watu wote watasema, "Amen!"

---

[a]**27:9** Kum 17:9; 26:18
[b]**27:12** Kum 11:29; Mwa 30:18; Yos 8:35; Amu 9:7
[c]**27:13** Kum 11:29
[d]**27:14** Kum 33:10; Yos 8:33; Neh 8:7-8; Dan 9:11; Mal 2:7-9
[e]**27:15** Kut 20:4; 34:17; 1Fal 11:5-7; 2Fal 23:13; Isa 44:9, 19; 66:3; Hes 5:22; 1Kor 14:6; Law 19:4; 26:1; Kum 4:16, 23; Isa 44:9; Hos 13:2; Hes 5:22; Yer 11:5
[f]**27:16** Mwa 31:35; Kut 21:12; Kum 5:16; Law 19:3
[g]**27:17** Kum 19:14; Mit 22:28
[h]**27:18** Law 19:14; Ay 29:15; Mit 28:10; Mt 15:14; Ufu 2:14
[i]**27:19** Kut 22:21; Kum 24:19; Kut 23:2; Kum 10:18; Mal 3:5
[j]**27:20** Mwa 34:5; Law 18:7; 1Kor 5:1
[k]**27:21** Kut 22:19; Law 8:23
[l]**27:22** Law 18:9; 20:17; 2Sam 13:1
[m]**27:23** Law 20:14
[n]**27:24** Mwa 4:23; Law 24:17; Kut 21:12; Hes 35:31
[o]**27:25** Kut 23:7-8; Law 19:16; Eze 22:12; Kum 10:17; 16:19; Za 15:5; Eze 22:12
[p]**27:26** Law 26:14; Kum 28:15; Za 119:21; Yer 11:3; Gal 3:10; Yer 11:5

*Baraka Za Utiifu*

### (Walawi 26:3-13; Kumbukumbu 7:12-24)

28 [a]Kama ukimtii BWANA Mungu wako
kwa bidii na kufuata amri zake zote
ninazokupa leo kwa bidii, BWANA Mungu
wako atakuweka juu ya mataifa yote katika
dunia. 2 [b]Baraka hizi zote zitakuja juu yako
na kukupata, kama ukimtii BWANA Mungu
wako:

3 [c]Utabarikiwa mjini na utabarikiwa
mashambani.
4 [d]Utabarikiwa uzao wa tumbo lako,
na mazao ya nchi yako na wanyama
wako wachanga wa kufugwa, yaani
ndama wa makundi yako ya ng'ombe,
na wana-kondoo wa makundi yako.
5 Kapu lako na vyombo vyako vya
kukandia vitabarikiwa.
6 [e]Utabarikiwa uingiapo na
utabarikiwa utokapo.

7 [f]BWANA atasababisha adui wainukao
dhidi yako kushindwa mbele yako.
Watakujia kwa njia moja lakini watakimbia
mbele yako kwa njia saba.
8 [g]BWANA ataagiza baraka juu ya ghala
zako na juu ya kila kitu utakachogusa
kwa mkono wako. BWANA Mungu wako
atakubariki katika nchi anayokupa.
9 [h]BWANA atakufanya kuwa taifa lake
takatifu, kama alivyokuahidi kwa kiapo,
kama ukishika maagizo ya BWANA
Mungu wako na kwenda katika njia zake.
10 [i]Kisha mataifa yote ya dunia wataona
kuwa unaitwa kwa jina la BWANA, nao
watakuogopa. 11 [j]BWANA atakupa kustawi
kwa wingi, katika tunda la uzao wa tumbo
lako, katika wanyama wachanga wa mifugo
yako na katika mazao ya ardhi yako, katika
nchi aliyowaapia baba zako kuwapa.
12 [k]BWANA atafungua mbingu, ghala zake
za baraka, kukupa mvua kwa majira yake
na kubariki kazi zako zote za mikono yako.
Utakopesha mataifa mengi lakini hutakopa
kwa yeyote. 13 [l]BWANA atakufanya kichwa,
wala si mkia. Kama utazingatia maagizo
ya BWANA Mungu wako ninayokupa siku
hii ya leo na kuyafuata kwa bidii, daima
utakuwa juu, kamwe hutakuwa chini.
14 [m]Usihalifu amri zangu zozote ninazokupa
leo, kwa kwenda kuume au kushoto, kwa
kufuata miungu mingine na kuitumikia.

*Laana Kwa Kutokutii*

### (Walawi 26:14-46)

15 [n]Hata hivyo, kama hutamtii BWANA
Mungu wako na kuzishika kwa bidii amri
zake zote na maagizo ninayokupa leo, laana
hizi zote zitakuja juu yako na kukupata:

16 Utalaaniwa mjini na utalaaniwa
mashambani.
17 Kapu lako na chombo chako cha
kukandia kitalaaniwa.
18 [o]Uzao wa tumbo lako utalaaniwa,
mazao ya ardhi yako, ndama wa
makundi yako ya ng'ombe na wana-
kondoo wa makundi yako.
19 Utalaaniwa uingiapo na utokapo.

20 [p]BWANA ataleta laana juu yako,
fadhaa na kukaripiwa katika kila kitu
unachokigusa kwa mkono wako, mpaka
uwe umeharibiwa na kuangamizwa ghafula

---

[a]**28:1** Kum 15:5; Law 26:3; Hes 24:7; Kum 26:19; Kut 15:26; Za 106:3; 111:10; Isa 1:19; 3:10; Yer 11:4; 12:16; 1Nya 14:2; Rum 2:10
[b]**28:2** Yer 32:24; Zek 1:6
[c]**28:3** Za 144:15; Mwa 39:5; Za 128:1-4
[d]**28:4** Mwa 49:25; Kum 8:18; Mit 10:22; 1Tim 4:8
[e]**28:6** Za 121:8
[f]**28:7** 2Nya 6:34; Law 26:8, 17
[g]**28:8** Kum 15:4
[h]**28:9** Kut 19:6; Law 26:3; Kum 7:6
[i]**28:10** Hes 6:27; 1Fal 8:43; Yer 25:29; Dan 9:18; 2Nya 7:14
[j]**28:11** Kum 30:9; Mwa 30:27; Mit 10:22
[k]**28:12** Ay 38:22; Za 135:7; Yer 10:13; 51:16; Za 65:11; 58:10; Yer 31:12; Law 26:4; 1Fal 8:35-36; 18:1; Za 104:13; Isa 5:6; 30:23; 32:20; 61:9; 65:23; Yer 32:38-41; Mal 3:12; Law 25:19; Kum 15:3-6; Eze 34:26
[l]**28:13** Yer 11:6; Kum 26:19
[m]**28:14** Kum 5:32; Yos 1:7
[n]**28:15** 1Fal 9:6; 2Nya 7:19; Kum 27:26; 27:26; Yos 23:15; 2Nya 12:5; Dan 9:11; Mal 2:2
[o]**28:18** Isa 3:1; Hab 3:17
[p]**28:20** Law 26:16; Yer 42:18; Mal 2:2; 3:9; 4:6; Za 39:11; 76:6; 80:16; Isa 17:13; 51:20; 54:9; 66:15; Eze 5:15; Kum 4:26; Kut 32:22

kwa ajili ya maovu uliyoyafanya kwa
kumwacha yeye. 21 [a]Bwana atakupiga kwa
magonjwa mpaka akuangamize kutoka nchi
unayoingia kuimiliki. 22 [b]Bwana atakupiga
kwa magonjwa ya kudhoofisha, kwa homa
na kuwashwa, hari na kwa ukame, kutu
na kuwa na uchungu ambavyo vitakupiga
mpaka uangamie.
23 [c]Anga juu yako itakuwa shaba, na
ardhi chini yako itakuwa chuma. 24 [d]Bwana
atafanya mvua ya nchi yako kuwa mavumbi
na mchanga; vitakujia kutoka angani mpaka
uangamie.
25 [e]Bwana atakufanya ushindwe mbele
ya adui zako. Utawajia kwa njia moja
lakini utawakimbia mbele yao kwa njia
saba, nawe utakuwa kitu cha kuchukiza
kwa falme zote za dunia. 26 [f]Mizoga yenu
itakuwa chakula cha ndege wa angani na
wanyama wa nchi, wala hapatakuwepo
mtu yeyote wa kuwafukuza. 27 [g]Bwana
atakupiga kwa majipu ya Misri na kwa
vidonda vitokavyo usaha na kuwashwa,
ambako huwezi kuponywa. 28 Bwana
atakupiga kwa wazimu, upofu na
kuchanganyikiwa kwa akili. 29 [h]Wakati wa
adhuhuri utapapasapapasa huku na huko
kama mtu kipofu katika giza. Hutafanikiwa
katika lolote ufanyalo; siku baada ya siku
utaonewa na kunyang’anywa, wala hakuna
yeyote atakayekuokoa.
30 [i]Utaposa mke, lakini mtu mwingine
atakutana naye kimwili. Utajenga nyumba,
lakini hutaishi ndani yake. Utapanda
shamba la mizabibu, lakini hutakula
matunda yake. 31 Ng’ombe wako atachinjwa
mbele ya macho yako lakini hutakula
nyama yake. Punda wako atachukuliwa kwa
nguvu kutoka kwako wala hatarudishwa.
Kondoo wako watapewa adui zako, wala
hakuna mtu yeyote wa kuwaokoa. 32 Wanao
na binti zako watatolewa kwa mataifa
mengine, nawe utayachosha macho yako
ukiwatazamia siku baada ya siku, hutakuwa
na nguvu kuinua mkono. 33 [j]Taifa usilolijua
watakula mazao ya nchi yako na taabu ya
kazi yako, hutakuwa na chochote, bali
kuonewa kikatili siku zako zote. 34 Vitu
utakavyoviona kwa macho yako vitakufanya
wazimu. 35 [k]Bwana atayapiga magoti yako
na miguu yako kwa majipu yenye maumivu
makali yasiyoponyeka, yakienea kutoka
nyayo za miguu yako hadi utosini.
36 [l]Bwana atakupeleka wewe na mfalme
uliyemweka juu yako uende kwenye taifa
ambalo hukulijua wewe wala baba zako.
Huko utaabudu miungu mingine, miungu
ya miti na mawe. 37 [m]Utakuwa kitu cha
kuchukiza, tena kitu cha kudharauliwa
na kudhihakiwa kwa mataifa yote huko
Bwana atakakokupeleka.
38 [n]Utapanda mbegu nyingi katika
shamba lakini utavuna haba, kwa sababu
nzige watazila. 39 [o]Utapanda mashamba ya
mizabibu na kuyapalilia, lakini hutakunywa
divai yake wala hutakusanya zabibu, kwa

---

[a]**28:21** Law 26:25; Hes 14:12; Yer 24:10; Amo 4:10
[b]**28:22** Kum 32:24; Law 26:16; 2Fal 8:1; Ay 12:15; Za 105:16; Yer 14:1; Hag 1:11; Mal 3:9; Hag 2:17; Law 26:25; Kum 4:26; Amo 4:9
[c]**28:23** Law 26:19
[d]**28:24** Law 26:19; Kum 11:17; 1Fal 8:35; 17:1; Isa 5:6; Yer 14:1; Hag 1:10
[e]**28:25** 1Sam 4:10; Za 78:62; Law 26:17; 2Nya 29:8; 30:7; Yer 15:4; 24:9; 26:6; 29:18; 44:12; Eze 23:46
[f]**28:26** Mwa 40:19; Za 79:2; Isa 18:6; Yer 7:33; 12:9; 15:2; 16:4; 19:7; 34:20
[g]**28:27** Kum 7:15; 1Sam 5:6
[h]**28:29** Mwa 19:11; Kut 10:21; Ay 5:14; 12:25; 24:13; 38:15; Isa 59:10; Amu 3:9; 2Fal 13:5; Es 4:14; Isa 19:20; 43:11; Hos 13:4; Oba 1:21
[i]**28:30** Ay 31:10; Isa 65:22; Amo 5:11; Yer 12:13; 8:10
[j]**28:33** Yer 5:15-17; Eze 25:4
[k]**28:35** Kum 7:15; Ufu 16:2; Ay 2:7; 7:5; 13:28; 30:17; Isa 1:6
[l]**28:36** 1Sam 12:25; Kum 4:27; 2Fal 24:14; 25:7-11; 2Nya 33:11; 36:21; Ezr 5:12; Yer 15:14; 16:13; 27:20; 29:1-9; 52:28; Mao 1:3; Kum 4:28
[m]**28:37** Yer 42:18; Eze 5:15; Za 22:7; 39:8; 44:13; 64:8; Yer 18:16; 48:27; Mik 6:16; 2Nya 7:20; Ezr 9:7; Yer 44:8; 1Fal 9:7; Za 44:14; Yer 19:8; 24:9; 25:9, 18; 29:18; Mao 2:15
[n]**28:38** Law 26:20; Za 129:7; Isa 5:10; Yer 12:13; Hos 8:7; Mik 6:15; Hag 1:6-9; 2:16; Kut 10:4; 10:15; Yoe 1:4
[o]**28:39** Law 10:9; Yoe 1:4; 2:25; Mal 3:11; Isa 5:10; 17:10-11; Sef 1:13

sababu wadudu watazila. 40 [a]Utakuwa na
mizeituni katika nchi yako yote, lakini
hutatumia hayo mafuta yake, kwa sababu
zeituni zitapukutika. 41 Utakuwa na wana
na binti lakini hawatakuwa nawe, kwa
sababu watachukuliwa mateka. 42 [b]Makundi
ya nzige yatavamia miti yako yote na mazao
ya nchi yako.

43 Mgeni anayeishi miongoni mwako
atainuka juu zaidi na zaidi kuliko wewe,
lakini wewe utashuka chini zaidi na
zaidi. 44 [c]Yeye atakukopesha, lakini wewe
hutamkopesha. Yeye atakuwa kichwa,
lakini wewe utakuwa mkia.

45 [d]Laana hizi zote zitakuja juu
yako. Zitakufuatia na kukupata mpaka
uangamizwe, kwa sababu hukumtii BWANA
Mungu wako, na kuzishika amri zake na
maagizo yake aliyokupa. 46 [e]Zitakuwa
ishara na ajabu kwako na kwa wazao
wako milele. 47 [f]Kwa sababu hukumtumikia
BWANA Mungu wako kwa furaha na kwa
moyo wakati wa kufanikiwa kwako, 48 [g]kwa
hiyo katika njaa na kiu, katika uchi na
umaskini wa kutisha, utawatumikia adui
ambao BWANA atawatuma dhidi yako. Yeye
ataweka nira ya chuma shingoni mwako
hadi amekwisha kukuangamiza.

49 [h]BWANA ataleta taifa dhidi yako kutoka
mbali, kutoka miisho ya dunia, kama tai
ashukiavyo mawindo chini, taifa ambalo
hutaijua lugha yake, 50 [i]taifa lenye uso mkali
lisilojali wazee wala kuwahurumia vijana.
51 [jk]Watakula wadogo wa mifugo yako na
mazao ya nchi yako mpaka umeangamia.
Hawatakuachia nafaka, divai mpya au
mafuta, wala ndama wowote wa kundi
lako au wana-kondoo wa kundi lako mpaka
umekuwa magofu. 52 [l]Nao wataizingira miji
yote katika nchi yako mpaka kuta ndefu za
ngome ambazo unazitegemea zimeanguka.
Watazingira miji yote katika nchi ambayo
BWANA Mungu wako anakupa.

53 [m]Utakula uzao wa tumbo lako, nyama
ya wana wako na binti zako ambao BWANA
Mungu wako amekupa, kwa sababu ya
mateso yale adui zako watakayokuletea
wakati wa kukuzingira. 54 Hata yule mtu
muungwana sana na makini miongoni
mwako hatakuwa na huruma kwa ndugu
yake mwenyewe au kwa mke ampendaye
au watoto wake waliosalia, 55 [n]naye
hatampa hata mmoja wao nyama ya
watoto wake ambao anawala. Kwa kuwa
hakuna kitu kingine kilichosalia kwake
katika mazingirwa makali ambayo adui
yako watakuletea kwa miji yako yote.
56 [o]Mwanamke ambaye ni muungwana sana
na makini miongoni mwako, yaani ambaye
ni makini sana na muungwana kiasi kwamba
asingethubutu kugusa ardhi kwa wayo wa
mguu wake, yeye atakuwa mchoyo kwa
mume ampendaye na mwanawe mwenyewe
au binti yake, 57 [p]kondoo wa nyuma kutoka
kwenye tumbo lake na watoto anaowazaa.
Kwa kuwa anakusudia kuwala kwa siri
wakati wa kuzingirwa na katika taabu zile
ambazo adui yako atazileta juu yako na
miji yako.

58 [q]Kama hutafuata kwa bidii maneno
yote ya sheria hii, ambayo yameandikwa
katika kitabu hiki na kama hutalicha hili

[a]**28:40** Yer 11:16; Mik 6:15
[b]**28:42** Amu 6:5; 7:12; Yer 46:23
[c]**28:44** Kum 26:19
[d]**28:45** Kut 15:9; Kum 4:25-26
[e]**28:46** Hes 16:38; Za 71:7; Isa 8:18; 20:3; Eze 5:15; Zek 3
[f]**28:47** Kum 10:12; Law 23:20; Neh 9:35; 9:35-37
[g]**28:48** Yer 14:3; Mao 4:4; Yer 28:13-14; Mwa 49:8; Isa 47:6; Yer 27:12; 28:14; Mt 11:29
[h]**28:49** Law 26:44; Isa 5:26-30; 7:18-20; 39:3; Yer 4:16; 5:15; 6:22; 25:32; 31:8; Hab 1:6; 2Sam 1:23; Yer 4:13; 48:40; 49:22; Mao 4:19; Eze 17:3; Hos 8:1; Mwa 11:7; 1Kor 14:21
[i]**28:50** Isa 47:6
[j]**28:51** Za 4:7; Isa 36:17; Hag 1:11; Hes 18:12; Amu 6:4
[k]**28:51** Isa 1:7; 62:8; Yer 5:15-17
[l]**28:52** 2Fal 6:24; Yer 10:18; Eze 1:10; Sef 1:14-17
[m]**28:53** Law 26:29; 2Fal 6:28-29; Mao 2:20; 4:10; Yer 19:9
[n]**28:55** 2Fal 6:29
[o]**28:56** Isa 47:1; Mao 4:10
[p]**28:57** Kum 28:53
[q]**28:58** Kum 31:24; Za 96:4; Yer 5:22; Mal 1:14; 2:5; 3:5, 16; 4:2; Kut 3:15; 6:3; Yos 7:9

jina la fahari na la kutisha, yaani la Bwana Mungu wako, [59] [a]Bwana ataleta mapigo ya kutisha juu yako na kwa wazao wako, maafa makali na ya kudumu, magonjwa mazito na ya kudumu. [60] [b]Atakuletea juu yako magonjwa yote ya Misri yale uliyoyaogopa, nayo yataambatana nawe. [61] [c]Pia Bwana atakuletea kila aina ya ugonjwa na maafa ambayo hayakuandikwa humu katika kitabu hiki cha sheria, mpaka utakapokuwa umeangamizwa. [62] [d]Ninyi ambao mlikuwa wengi kama nyota za angani mtaachwa wachache tu, kwa sababu hamkumtii Bwana Mungu wenu. [63] [e]Kama ilivyompendeza Bwana kuwafanya ninyi mstawi na kuongezeka kwa idadi, ndivyo itakavyompendeza kuwaharibu na kuwaangamiza ninyi. Mtang'olewa kutoka nchi mnayoiingia kuimiliki.

[64] [f]Kisha Bwana atawatawanya miongoni mwa mataifa yote, kutoka mwisho mmoja wa dunia hadi mwingine. Huko mtaabudu miungu mingine, miungu ya miti na ya mawe, ambayo ninyi wala baba zenu hamkuijua. [65] [g]Miongoni mwa mataifa hayo hamtapata raha wala mahali pa kupumzisha wayo wa mguu wenu. Huko Bwana atawapa mahangaiko ya mawazo, macho yaliyochoka kwa kungojea na moyo uliokata tamaa. [66] Utaishi katika mahangaiko siku zote, ukiwa umejaa hofu usiku na mchana, wala hutakuwa kamwe na uhakika wa maisha yako. [67] [h]Wakati wa asubuhi utasema hivi, "Laiti ingekuwa jioni!" Jioni utasema, "Laiti ingekuwa asubuhi," kwa sababu ya hofu ile itakayojaza moyo wako na vitu vile macho yako yatakavyoviona. [68] [i]Bwana atawarudisha tena Misri kwa meli, safari niliyosema kamwe hamngeenda tena. Huko mtajiuza ninyi wenyewe kwa adui zenu kama watumwa wa kiume na wa kike, lakini hakuna yeyote atakayewanunua.

### *Kufanya Upya Agano*

**29** [j]Haya ndiyo maneno ya Agano Bwana aliyomwagiza Mose kufanya na Waisraeli huko Moabu, kuwa nyongeza ya Agano alilofanya nao huko Horebu.

[2] [k]Mose akawaita Waisraeli wote akawaambia:

Macho yenu yameona yale yote Bwana aliyofanya kwa Mfalme Farao huko Misri, kwa maafisa wake wote na kwa nchi yake yote. [3] [l]Kwa macho yenu wenyewe mliona yale majaribu makubwa, ishara zile za miujiza na maajabu makubwa. [4] [m]Lakini mpaka leo Bwana hajawapa akili ya kuelewa au macho yanayoona au masikio yanayosikia. [5] [n]Kwa muda wa miaka arobaini niliyowaongoza jangwani, nguo zenu hazikuchakaa, wala viatu miguuni mwenu. [6] [o]Hamkula mkate na hamkunywa divai wala kileo chochote. Nilifanya hivi ili mpate kujua kuwa mimi ndimi Bwana Mungu wenu.

[7] [p]Wakati mlipofika mahali hapa, Sihoni mfalme wa Heshboni na Ogu mfalme wa Bashani walikuja kupigana dhidi yetu, lakini tuliwashinda. [8] [q]Tuliichukua nchi yao

---

[a]**28:59** 1Fal 9:7, 9; Mao 1:9, 12; 4:12; Dan 9:12; 2Nya 21:12-15
[b]**28:60** Kut 15:26
[c]**28:61** Kum 29:21; 30:10; 31:26; Yos 1:8; 8:34; 23:6; 24:26; 2Fal 14:6; 22:8; 2Nya 17:9; 25:4; Neh 8:1, 18; Mal 4:4; Kum 4:25-26
[d]**28:62** Mwa 22:17; Kum 4:27; 10:22; Law 26:22; Neh 9:23
[e]**28:63** Kum 30:9; Isa 62:5; 65:19; Yer 32:41; Sef 3:17; Mit 1:26; Mwa 6:7; Za 52:5; Yer 12:14; 31:28; 45:4
[f]**28:64** Kum 4:27; Ezr 9:7; Isa 6:12; Yer 32:23; 43:11; 52:27; Za 44:11; Neh 1:8; Yer 13:24; 18:17; 22:22; Kum 4:32; Yer 8:19; Kum 11:28; 32:17; Law 26:33
[g]**28:65** Mao 1:3; Ay 11:20; Law 26:16, 30; Hos 9:17
[h]**28:67** Ay 7:4
[i]**28:68** Kut 13:14; Yer 44:7; Hos 8:13; 9:3
[j]**29:1** Law 7:38; Kut 3:1; Kum 5:2-3
[k]**29:2** Kut 19:4
[l]**29:3** Kum 4:34; 7:19
[m]**29:4** Isa 6:10; 32:3; 48:8; Yer 5:21; Eze 12:2; Mt 13:15; Rum 11:8; Efe 4:18; Mdo 28:26-27; Za 13:3; 19:8; Yn 8:43; Efe 1:18; 2The 2:11
[n]**29:5** Kum 8:2-4
[o]**29:6** Law 10:9; Kum 8:4; Kut 16:12; Neh 9:15; Za 78:24
[p]**29:7** Hes 21:25-26; 21:21-24, 33-35; Kum 2:26–3:11
[q]**29:8** Za 78:55; 135:12; 136:22; Hes 32:33; Kum 3:12-13

na kuwapa Wareubeni, Wagadi na nusu ya
kabila la Manase kama urithi wao.
9 [a]Fuateni kwa bidii masharti ya Agano
hili, ili kwamba mweze kustawi katika
kila kitu mnachofanya. 10 Ninyi nyote leo
mnasimama mbele za BWANA Mungu wenu;
mkiwa viongozi na wakuu wenu, wazee
na maafisa wenu, na wanaume wengine
wote wa Israeli, 11 [b]pamoja na watoto
wenu, wake zenu na pia wageni waishio
katika kambi zenu wanaowapasulia kuni
na kuwachotea maji. 12 Mnasimama hapa
ili kufanya Agano na BWANA Mungu wenu,
Agano ambalo Mungu analifanya nanyi siku
hii ya leo na kulitia muhuri kwa kiapo,
13 [c]kuwathibitisha ninyi siku hii ya leo kama
taifa lake, ili aweze kuwa Mungu wenu
kama alivyowaahidi na kama alivyowaapia
baba zenu Abrahamu, Isaki na Yakobo.
14 [d]Ninafanya Agano hili pamoja na kiapo
chake, sio na ninyi tu 15 [e]mnaosimama hapa
na sisi leo mbele za BWANA Mungu wetu,
bali pia pamoja na wale ambao hawapo
hapa leo.
16 Ninyi wenyewe mnajua jinsi tulivyoishi
nchini Misri na jinsi tulivyopita katikati
ya nchi mpaka tukafika hapa. 17 [f]Mliona
miongoni mwao vinyago vyao vya
kuchukiza na sanamu za miti na mawe, za
fedha na dhahabu. 18 [g]Hakikisheni kwamba
hakuna mwanaume au mwanamke, ukoo au
kabila miongoni mwenu leo ambalo moyo
wake utamwacha BWANA Mungu wetu,
kwenda kuabudu miungu ya mataifa hayo.
Hakikisheni hakuna mzizi miongoni mwenu
unaotoa sumu chungu ya namna hii.
19 [h]Wakati mtu wa namna hii asikiapo
maneno ya kiapo hiki, hujibariki
mwenyewe na kisha hufikiri, “Nitakuwa
salama, hata kama nikiendelea kuifuata
njia yangu mwenyewe.” Hili litaleta maafa
juu ya nchi iliyonyeshewa sawasawa na
nchi kame. 20 [i]BWANA kamwe hatakuwa
radhi kumsamehe, ghadhabu na wivu
wa Mungu vitawaka dhidi ya mtu huyo.
Laana zote zilizoandikwa katika kitabu
hiki zitamwangukia na BWANA atafuta jina
lake chini ya mbingu. 21 [j]BWANA atamtwaa
peke yake kutoka makabila ya Israeli kwa
maangamizo, kulingana na laana zote za
Agano zilizoandikwa kwenye Kitabu hiki
cha Sheria.
22 [k]Watoto wako watakaofuata baada
yako katika vizazi vya baadaye na wageni
ambao watakuja kutoka nchi za mbali,
wataona maafa, yaliyoipata nchi na
magonjwa ambayo BWANA aliyaleta juu
yake. 23 [l]Nchi yote itakuwa jaa linaloungua
la chumvi na kiberiti: hakutakuwa
kilichopandwa, hakutakuwa kinachochipua,
wala hakutakuwa mimea inayoota juu
yake. Itakuwa kama maangamizo ya
Sodoma na Gomora, Adma na Seboimu,
ambazo BWANA aliangamiza kwa hasira
kali. 24 [m]Mataifa yote yatauliza: “Kwa nini
BWANA amefanya hivi juu ya nchi hii? Kwa
nini hasira hii kali ikawaka?”
25 [n]Na jibu litakuwa: “Ni kwa sababu
watu hawa waliacha Agano la BWANA,
Mungu wa baba zao, Agano alilofanya
nao wakati alipowatoa katika nchi ya
Misri. 26 Walienda zao na kuabudu miungu
mingine na kuisujudia, miungu wasioijua,
miungu ambayo Mungu hakuwapa. 27 [o]Kwa
hiyo hasira ya BWANA ikawaka dhidi ya
nchi hii, hivyo Mungu akaleta juu yake
laana zote zilizoandikwa katika kitabu hiki.

[a]**29:9** Kum 4:6; Yos 1:7; Kut 19:5; Za 25:10; 103:18; 2Nya 31:21; 1Fal 2:3; Yos 1:8
[b]**29:11** Yos 9:21, 23, 27; 1Nya 20:3
[c]**29:13** Mwa 6:18; Kut 6:7; 19:6; Mwa 17:7
[d]**29:14** Kut 19:5; Isa 59:21; Yer 31:31; 32:40; 50:5; Eze 16:62; 37:26; Ebr 8:7-8
[e]**29:15** Mwa 6:18; Mdo 2:39
[f]**29:17** Kut 20:23; Kum 4:28; 28:36
[g]**29:18** Kum 13:6; 11:16; Ebr 12:15
[h]**29:19** Za 72:17; Isa 65:16; Za 36:2; 14:1; Hes 15:39; Yer 7:24; Ay 15:16; 34:7; Efe 4:19
[i]**29:20** Kut 23:21; 34:4; Eze 23:25; Sef 1:18; Za 74:1; 79:5; 80:4; Eze 36:5; 2Fal 13:23; 14:27; Ufu 3:5; Kut 32:33
[j]**29:21** Kum 28:61; 32:23; Eze 7:26; Mt 24:51
[k]**29:22** Yer 19:8; 49:17; 50:13
[l]**29:23** Isa 1:7; 6:11; 9:18; 64:10; Yer 12:11; 44:2; 6; Mik 5:11; Mwa 13:10; Eze 47:11; Mwa 19:24-25; Sef 2:9; Mt 10:15; Rum 9:29; Mwa 14:8; Yer 17:6
[m]**29:24** 1Fal 9:6; 2Nya 36:19; Yer 16:10; 22:8-9; 52:13
[n]**29:25** 2Fal 17:23; 2Nya 36:21
[o]**29:27** Kum 28:15; Dan 9:11-14

28 [a]Katika hasira kali na katika ghadhabu
kuu BWANA aliwang'oa kutoka nchi yao na
kuwasukumia katika nchi nyingine, kama
ilivyo sasa."
29 [b]Mambo ya siri ni ya BWANA Mungu
wetu, bali yaliyofunuliwa ni yetu na watoto
wetu milele, ili tuweze kuyafanya maneno
yote ya sheria hii.

*Mafanikio Baada Ya Kumgeukia Bwana*

30 [c]Wakati baraka hizi zote pamoja
na laana nilizoziweka mbele yako
zitakapokujia, nawe ukazitafakari
moyoni popote BWANA Mungu wako
atakapokutawanya miongoni mwa
mataifa, 2 [d]hapo wewe na watoto wako
mtakapomrudia BWANA Mungu wako,
na kumtii kwa moyo wako wote na kwa
roho yako yote kulingana na kila kitu
ninachokuamuru leo, 3 [e]ndipo BWANA
Mungu wako atakapokurudisha kutoka
utumwani na kukuhurumia, naye
atakukusanya tena kutoka mataifa yote kule
alikutawanya. 4 [f]Hata kama umefukuziwa
katika nchi ya mbali kiasi gani chini ya
mbingu, kutoka huko BWANA Mungu
wako atakukusanya na kukurudisha.
5 [g]Yeye BWANA atakurudisha katika
nchi iliyokuwa mali ya baba zako, nawe
utaimiliki. Naye atakufanya ufanikiwe sana
na kukuzidisha kwa idadi kuliko baba zako.
6 [h]BWANA Mungu wako ataitahiri mioyo
yenu na mioyo ya wazao wenu ili mweze
kumpenda kwa moyo wako wote na kwa
roho yako yote ukaishi. 7 [i]BWANA Mungu
wako ataweka laana hizi zote juu ya adui
zako ambao wanakuchukia na kukutesa.
8 Utamtii tena BWANA na kuzishika amri
zake zote ninazokupa leo. 9 [j]Ndipo BWANA
Mungu wako atakapokufanikisha sana
katika kazi zote za mikono yako na katika
uzao wa tumbo lako, wadogo wa mifugo
yako na mazao ya nchi yako. BWANA
atakufurahia tena na kukufanikisha, kama
alivyowafurahia baba zako, 10 [k]kama
ukimtii BWANA Mungu wako, na kuzishika
amri zake na maagizo yake ambayo
yameandikwa katika Kitabu hiki cha Sheria,
na kumgeukia BWANA Mungu wako kwa
moyo wako wote na kwa roho yako yote.

*Uzima Na Mauti*

11 [l]Ninachokuagiza leo sio kigumu sana
kwako au usichokiweza. 12 [m]Hakiko juu
mbinguni, ili uulize, "Ni nani atakayepanda
mbinguni kukileta na kututangazia ili
tuweze kutii?" 13 [n]Wala hakiko ng'ambo
ya bahari, ili uulize, "Ni nani atakayevuka
bahari kwenda kukichukua na kututangazia
ili tupate kutii?" 14 [o]La hasha! Lile neno liko
karibu sana nawe; liko kinywani mwako
na ndani ya moyo wako ili uweze kulitii.
15 [p]Tazama, naweka mbele yako leo
uzima na mafanikio, mauti na maangamizo.
16 [q]Ninakuamuru leo kwamba umpende
BWANA Mungu wako, utembee katika
njia zake, na kutunza maagizo yake,
amri na sheria zake; ndipo utakapoishi
na kuongezeka, naye BWANA Mungu

[a]**29:28** Za 7:11; 1Fal 14:15; 2Nya 7:20; Za 9:6; 52:5; Mit 2:22; Yer 12:14; 31:28; 42:10; Eze 19:12
[b]**29:29** Mdo 1:7; Yn 5:39; Mdo 17:11; 2Tim 3:16; Ay 11:6; 7; Mit 3:32; Yer 23:18; Amo 3:7; Za 19:7; Lk 16:29; 2Tim 3:16; Mdo 17; 11
[c]**30:1** Kum 11:26; Law 26:40-45; Kum 4:32; 29:28; 1Fal 8:47
[d]**30:2** Kum 4:29-30
[e]**30:3** Za 14:7; 53:6; 85:1; 126:4; Yer 30:18; 33:11; Eze 16:53; Yoe 3:1; Sef 2:7; Kum 13:17; Mwa 48:21; 11:4; Kum 4:27; Isa 11:11; Yer 12:15; 16:15; 26:4; 29:14; 48:47; 49:6
[f]**30:4** Isa 17:6; 24:13; 27:12; 40:11; 41:5; 49:5; 56:8; Eze 20:34, 41; 34:13; Za 19:6; Neh 1:8-9; Isa 11:12; 42:10; 43:6; 48:20; 62:11; Yer 31:8, 10; 50:2
[g]**30:5** Yer 29:14; Kum 7:13
[h]**30:6** Kum 6:24; 10:16; 6:5; Yer 32:29
[i]**30:7** Mwa 12:3; Kum 7:15
[j]**30:9** Yer 1:10; 24:6; 31:28; 32:41; 42:10; 45:4; Kum 28:63; Eze 34:27; Yer 32:41; 33:9; Sef 3:17; Lk 15:6, 10, 32; Yn 15; 11
[k]**30:10** Kum 28:61; 4:29
[l]**30:11** Za 19:8; Isa 45:19-23; 63:1
[m]**30:12** Mit 30:4; Rum 10:6; Yn 3:13
[n]**30:13** Ay 28:14; Rum 10:7
[o]**30:14** Kum 6:6; Rum 10:8
[p]**30:15** Mit 10:16; 11:9; 12:28; 3:1-2; Kum 28:11; Za 25:13; 106:5; Mwa 2:17; Kum 11:26
[q]**30:16** Kum 6:5; 4:1; 32:17; Neh 9:29

wako atakubariki katika nchi unayoingia
kuimiliki.
17 Lakini kama moyo wako ukigeukia
mbali ukawa huna utii, kama umevutwa
kuisujudia miungu mingine na kuiabudu,
18 [a]nakutangazia leo hii kwamba hakika
utaangamizwa. Hutaishi maisha marefu
katika nchi unayovuka Yordani kuiingia
na kuimiliki.
19 [b]Leo ninaziita mbingu na nchi kama
mashahidi dhidi yako kwamba nimeweka
mbele yako uzima na mauti, baraka na
laana. Basi sasa chagueni uzima, ili wewe
na watoto wako mpate kuishi, 20 [c]na ili
upate kumpenda BWANA Mungu wako,
uisikilize sauti yake na kuambatana naye.
Kwa kuwa BWANA ndiye uzima wako, na
atakupa wingi wa siku ili upate kuishi
katika nchi aliyoapa kuwapa baba zako
Abrahamu, Isaki na Yakobo.

*Yoshua Kutawala Baada Ya Mose*

**(Hesabu 27:12-23)**

31 Kisha Mose akaenda akasema maneno
haya kwa Waisraeli wote: 2 [d]"Sasa nina
miaka mia moja na ishirini nami siwezi
tena kuwaongoza. BWANA ameniambia,
'Hutavuka Yordani.' 3 [e]BWANA Mungu
wenu, yeye mwenyewe atavuka mbele yenu.
Ataangamiza mataifa haya mbele yenu, nanyi
mtaimiliki nchi yao. Pia Yoshua atavuka
mbele yenu, kama BWANA alivyosema.
4 [f]Naye BWANA atawafanyia watu hao kile
alichowafanyia Sihoni na Ogu, wafalme wa
Waamori, ambao aliwaangamiza pamoja
na nchi yao. 5 [g]BWANA atawakabidhi
kwenu, nanyi lazima mwatendee yale yote
niliyowaamuru. 6 [h]Kuweni imara na moyo
wa ushujaa. Msiogope wala msifadhaike
kwa sababu yao, kwa kuwa BWANA Mungu
wenu anakwenda pamoja nanyi; kamwe
hatawaacha wala hatawatupa ninyi."
7 [i]Kisha Mose akamwita Yoshua na
akamwambia mbele ya Israeli wote, "Uwe
imara na moyo wa ushujaa, kwa kuwa ni
lazima uende na watu hawa katika nchi
ile BWANA aliyowaapia baba zao kuwapa,
nawe ni lazima uwagawie kama urithi
wao. 8 [j]BWANA mwenyewe atakutangulia
naye atakuwa pamoja nawe; kamwe
hatakuacha wala hatakutupa. Usiogope,
wala usifadhaike."

*Kusoma Sheria*

9 [k]Kwa hiyo Mose akaandika sheria hii
na kuwapa makuhani, wana wa Lawi,
waliochukua Sanduku la Agano la BWANA
na wazee wote wa Israeli. 10 [l]Kisha Mose
akawaamuru, akasema: "Mwishoni
mwa kila miaka saba, katika mwaka wa
kufuta madeni, wakati wa Sikukuu ya
Vibanda, 11 [m]Waisraeli wote wanapokuja
mbele za BWANA Mungu wenu mahali
atakapopachagua, utasoma sheria hii
mbele yao masikioni mwao. 12 [n]Kusanya
watu wote, wanaume, wanawake, watoto
na wageni wanaoishi katika miji yenu,
ili waweze kusikia na kujifunza kumcha
BWANA Mungu wenu na kufuata kwa bidii
maneno yote ya sheria hii. 13 [o]Watoto wao,
ambao hawaijui sheria hii, lazima waisikie
na kujifunza kumcha BWANA Mungu

[a]**30:18** Kum 8:19
[b]**30:19** Kum 4:26; 11:26
[c]**30:20** Kum 6:5; 4:1; 8:3; 32:47; 10:20; Za 27:1; Yn 5:26; Mdo 17:28; Mit 3:22; Mwa 12:7; Za 37:3
[d]**31:2** Kut 7:7; Hes 27:17; Kum 34:7; 1Fal 3:7; Kum 3:23-26
[e]**31:3** Hes 27:18; Kum 9:3; 7:1; 3:28
[f]**31:4** Hes 21:33
[g]**31:5** Kum 2:33; 7:2
[h]**31:6** Yos 1:6-9, 18; 10:23; 1Nya 22:13; 28:20; 2Nya 32:7; Yer 1:8, 17; Eze 2:6; Mwa 28:15; Kum 1:29; 20:4; Mt 28:20; Za 56:9; 118:6; Kum 4:31; 1Sam 12:22; 1Fal 6:13; Za 94:14; Isa 41:17; Ebr 13:5
[i]**31:7** Hes 27:23; Yos 1:6; Kum 1:38; 3:28
[j]**31:8** Kut 13:21; Mwa 28:15; Kut 33:14; Kum 4:31
[k]**31:9** Kut 17:14; Hes 4:15; 1Nya 15:2
[l]**31:10** Kum 15:1; Kut 23:16; Kum 16:13; Law 23:34
[m]**31:11** Kum 16:16; 12:5; Yos 8:34-35; 2Fal 23:2; Neh 8:2
[n]**31:12** Kum 4:10; Hag 1:12; Mal 1:6; 3:5, 16
[o]**31:13** Kum 11:2; Za 78:6-7; Mit 22:6; Efe 6:4

wenu kwa muda mtakaoishi katika nchi
mnayovuka Yordani kuimiliki.”

*Kuasi Kwa Waisraeli Kunatabiriwa*

14 [a]BWANA akamwambia Mose, “Sasa
siku ya kifo chako imekaribia. Mwite
Yoshua, mkajihudhurishe katika Hema la
Kukutania, mahali nitakapompa maagizo ya
kazi.” Kwa hiyo Mose na Yoshua wakaja na
kujihudhurisha kwenye Hema la Kukutania.
15 [b]Kisha BWANA akatokea katika Hema
katika nguzo ya wingu, nalo wingu
likasimama juu ya ingilio la Hema. 16 [c]Kisha
BWANA akamwambia Mose: “Unakwenda
kupumzika na baba zako, nao watu hawa
hivi karibuni watazini na miungu migeni
ya nchi wanayoingia. Wataniacha na
kuvunja Agano nililofanya nao. 17 [d]Siku hiyo
nitawakasirikia na kuwaacha; nitawaficha
uso wangu, nao wataangamizwa. Maafa
mengi na shida nyingi zitakuja juu yao,
nao siku hiyo watauliza, ‘Je, maafa haya
hayakuja juu yetu kwa sababu Mungu
wetu hayuko pamoja nasi?’ 18 Nami hakika
nitauficha uso wangu siku hiyo kwa sababu
ya maovu yao yote kwa kugeukia miungu
mingine.
19 [e]“Sasa ujiandikie wimbo huu,[f]
uwafundishe Waisraeli na uwaamuru
wauimbe, ili upate kuwa ushahidi wangu
dhidi yao. 20 [g]Nitakapokwisha kuwaingiza
katika nchi itiririkayo maziwa na asali, nchi
niliyowaahidi baba zao kwa kiapo, nao
watakapokula wakashiba na kufanikiwa,
watageukia miungu mingine na kuiabudu,
wakinikataa mimi na kuvunja Agano langu.
21 [h]Maafa na shida zitakapokuja juu yao,
wimbo huu utashuhudia dhidi yao, kwa
sababu hautasahauliwa na wazao wao.
Ninajua lile wanaloandaa kufanya, hata
kabla sijawaingiza katika nchi niliyowaahidi
kwa kiapo.” 22 Hivyo Mose akaandika
wimbo huu siku ile na akawafundisha
Waisraeli.
23 [i]BWANA akampa Yoshua mwana wa
Nuni agizo hili: “Uwe hodari na shujaa,
kwa kuwa utawaleta Waisraeli katika nchi
niliyowaahidi kwa kiapo, nami mwenyewe
nitakuwa pamoja nawe.”
24 [j]Baada ya Mose kumaliza kuandika
kwenye kitabu maneno ya sheria hii
kutoka mwanzo hadi mwisho, 25 akawapa
Walawi wale waliolibeba Sanduku la
Agano la BWANA agizo hili, akawaambia:
26 “Chukueni Kitabu hiki cha Sheria
mkakiweke kando ya Sanduku la Agano
la BWANA Mungu wenu. Hapo ndipo
kitakapokaa kama shahidi dhidi yenu.
27 [k]Kwa kuwa ninajua jinsi mlivyo waasi na
mlivyo na shingo ngumu. Kama mmekuwa
mkiasi dhidi ya BWANA nikiwa bado niko
hai na nikiwa pamoja nanyi, mtaasi mara
ngapi baada ya kufa kwangu! 28 [l]Kusanyeni
mbele yangu wazee wote wa makabila yenu
na maafisa wenu wote, ili nipate kusema
maneno haya masikioni mwao na kuziita
mbingu na nchi ili kushuhudia dhidi
yao. 29 [m]Kwa kuwa ninajua baada ya kifo
changu hakika mtakuwa waovu kabisa na
kugeuka kutoka njia niliyowaamuru ninyi.
Katika siku zijazo, maafa yatawapata kwa

---

[a]**31:14** Mwa 25:8; Hes 27:13; 23; Kum 34:9; Yos 1:1-9; Hes 27:19; Kut 33:9-11
[b]**31:15** Kut 33:9; Za 99:7
[c]**31:16** Mwa 15:15; Kut 34:15; Kum 4:25-28; Amu 2:12; 10:6-13; 1Fal 9:9; 18:18; 19:10; Yer 2:13; 5:19; 19:4; 2Sam 7:12; 2Fal 22:16, 17; Isa 1:4
[d]**31:17** Kum 32:16; Amu 2:14; 20; 10:7; 2Fal 13:3; 22:13; Za 106:29, 40; Yer 7:18; 21:5; 36:17; Amu 6:13; 2Nya 15:2; 24:20; Ezr 8:22; Za 44:9; Isa 2:6; Kum 32:20; Isa 1:15; 45:15; 53:3; 54:8; Ay 13:24; Za 13:1; 27:9; 30:7; 104:29; Isa 50:6; Yer 33:5; Eze 39:29; Mik 3:4; Yer 4:20; Eze 7:26; Hes 14:42; Hos 9:12
[e]**31:19** Mwa 31:50
[f]19 Wimbo huu hapa ina maana wimbo wa Mose.
[g]**31:20** Kum 6:10-12; Za 4:2; 16:4; 40:4; Yer 13:25; Dan 3:28; Amo 2:4; Kum 8:19; 11:16-17
[h]**31:21** Kum 4:30; 1Nya 28:9; Hos 5:3; Yn 2:24-25
[i]**31:23** Yos 1:6
[j]**31:24** Kum 17:18; 2Fal 22:8; Kum 28:58
[k]**31:27** Kut 23:21; 32:9; Kum 9:27; 2Nya 30:8; Za 78:8; Isa 48:4; Za 32
[l]**31:28** Kum 4:26; 30:19; 32:1; Ay 20:27; Isa 26:21
[m]**31:29** Kum 4:16; Ufu 9:20; 1Fal 9:9; 22:23; 2Fal 22:16

sababu mtafanya maovu mbele ya macho ya BWANA, na kuchochea hasira yake kwa yale mikono yenu itakayokuwa imefanya."

*Wimbo Wa Mose*

30 Mose akayasoma maneno ya wimbo huu kutoka mwanzo hadi mwisho katika masikio ya kusanyiko lote la Israeli:

32 [a]Sikilizeni, enyi mbingu, nami nitasema;
sikia, ee nchi, maneno ya kinywa changu.
2 [b]Mafundisho yangu na yanyeshe kama mvua,
na maneno yangu na yashuke kama umande,
kama manyunyu juu ya majani mabichi,
kama mvua tele juu ya mimea myororo.

3 [c]Nitalitangaza jina la BWANA.
Naam, sifuni ukuu wa Mungu wetu!
4 [d]Yeye ni Mwamba, kazi zake ni kamilifu,
njia zake zote ni haki.
Mungu mwaminifu ambaye hakosei,
yeye ni mnyofu na mwenye haki.

5 [e]Wamefanya mambo ya upotovu mbele zake;
kwa aibu yao, wao si watoto wake tena,
lakini ni kizazi kilicho kiovu na kilichopotoka.
6 [f]Je, hii ndiyo njia ya kumlipa BWANA,
enyi watu wajinga na wasio na busara?
Je, yeye siye Baba yenu, Muumba wenu,
aliyewafanya ninyi na kuwaumba?

7 [g]Kumbuka siku za kale;
tafakari vizazi vya zamani vilivyopita.
Uliza baba yako, naye atakuambia,
wazee wako, nao watakueleza.
8 [h]Aliye Juu Sana alipowapa mataifa urithi wao,
alipogawanya wanadamu wote,
aliweka mipaka kwa ajili ya mataifa
sawasawa na hesabu ya wana wa Israeli.
9 [i]Kwa kuwa fungu la BWANA ni watu wake,
Yakobo kura yake ya urithi.

10 [j]Katika nchi ya jangwa alimkuta,
katika nyika tupu ivumayo upepo.
Alimhifadhi na kumtunza;
akamlinda kama mboni ya jicho lake,
11 [k]kama tai avurugaye kiota chake,
na kurukaruka juu ya makinda yake,
ambaye hutanda mabawa yake kuwadaka,
na huwachukua kwenye mabawa yake.

---

[a]**32:1** Za 49:1; Mik 1:2; Yer 2:12; Kum 4:26; Isa 1:2
[b]**32:2** 2Sam 23:4; Za 107:20; Isa 9:8; 55:11; Mik 5:7; Za 65:10; 68:9; 72:8; 147:8
[c]**32:3** Za 118:17; 145:6; Kut 33:16-19; 34:4-6; Kum 3:24
[d]**32:4** Mwa 49:24; 2Sam 22:31; Za 18:30; 19:7; Kum 4:35; Za 92:15; Mwa 18:25
[e]**32:5** Kum 31:29; Mt 17:17; Lk 9:41; Mdo 2:40
[f]**32:6** Za 116:12; 94:8; Yer 5:21; Kut 4:22; 2Sam 7:24; Isa 63:16
[g]**32:7** Za 44:1; 74:2; 74:2; 77:5; Isa 51:9; 63:9; Kum 4:32; Yos 8:8; 20:4; Za 78:4; Isa 46:9; Kut 10:2; 13:14; Ay 15:18
[h]**32:8** Za 7:8; Mwa 11:8; Mdo 8:1; Za 74:17; Hes 23:9; Kum 33:12; 28; Yer 23:6; Mdo 17:26
[i]**32:9** Za 16:5; 73:26; 119:57; 142:5; Yer 10:16; Kum 9:29; 1Sam 26:19; 1Fal 8:51-53
[j]**32:10** Kum 1:19; 8:15; Ay 12:24; Za 107:40; 32:10; Yer 31:22; Za 17:8; Mit 7:2; Hos 13:5; Zek 2:8
[k]**32:11** Kut 19:4; Za 17:8; 18:10-19; 61:4

12 [a]BWANA peke yake alimwongoza;
hakuwepo mungu mgeni pamoja naye.

13 [b]Akamfanya apande sehemu zilizoinuka za nchi,
akamlisha kwa mavuno ya mashamba.
Akamlea kwa asali toka mwambani,
na kwa mafuta kutoka mwamba mgumu,
14 [c]kwa jibini na maziwa kutoka makundi ya ng'ombe
na kutoka makundi ya mbuzi,
kwa mafuta ya wana-kondoo na mbuzi,
kwa kondoo dume wazuri wa Bashani,
na kwa ngano nzuri.
Ukanywa damu ya zabibu inayotoa povu.

15 [d]Yeshuruni[e] alinenepa na kupiga teke;
alikuwa na chakula tele,
akawa mzito na akapendeza sana.
Akamwacha Mungu aliyemuumba,
na kumkataa Mwamba Mwokozi wake.
16 [f]Wakamfanya Mungu kuwa na wivu kwa miungu yao migeni,
na kumkasirisha kwa sanamu zao za machukizo.
17 [g]Wakatoa dhabihu kwa pepo, ambao si Mungu:
miungu wasiyoijua,
miungu iliyojitokeza siku za karibuni,
miungu ambayo baba zenu hawakuiogopa.
18 [h]Mkamwacha Mwamba, aliyewazaa ninyi;
mkamsahau Mungu aliyewazaa.

19 [i]BWANA akaona hili, akawakataa,
kwa sababu alikasirishwa
na wanawe na binti zake.
20 [j]Akasema, "Nitawaficha uso wangu,
nami nione mwisho wao utakuwa nini,
kwa kuwa wao ni kizazi kilichopotoka,
watoto ambao si waaminifu.
21 [k]Wamenifanya niwe na wivu
kwa kile ambacho si mungu,
na kunikasirisha kwa sanamu zao
zisizokuwa na thamani.
Nitawafanya wawaonee wivu wale ambao si taifa.
Nitawafanya wakasirishwe
na taifa lile lisilo na ufahamu.
22 [l]Kwa maana moto umewashwa kwa hasira yangu,
ule uwakao hadi kwenye vina vya mauti.
Utateketeza dunia pamoja na mazao yake,
na kuwasha moto katika misingi ya milima.

---

[a]**32:12** Za 106:9; Isa 63:13; Yer 31:32; Kum 4:35; Amu 2:12; Za 18:31; 81:9; Isa 43:12; 45:5
[b]**32:13** Kum 33:29; 2Sam 22:34; Za 18:33; Isa 33:16; 58:14; Eze 36:2; Ebr 3:19; Kum 8:8; 33:24; Ay 29:6
[c]**32:14** Hes 21:33; Za 65:9; 81:16; 147:14; Mwa 49:11
[d]**32:15** Kum 33:5; 26; Isa 44:2; Kum 31:20; Yer 5:28; Kum 31:16; Isa 1:4, 28; 58:2; 65:11; Yer 15:6; Eze 14:5; Mwa 49:24
[e]15 Yeshuruni maana yake ni Yeye aliye mnyofu, yaani Israeli (ona pia Kum 33:26; Isa 44:2).
[f]**32:16** 1Kor 10:22; Kum 31:17; 1Fal 14:9
[g]**32:17** Kut 32:8; 22:20; 1Kor 10:20; Kum 28:64; Amu 5:8
[h]**32:18** Amu 3:7; 1Sam 12:9; Za 44:17, 20; 106:21; Yer 2:32; Eze 23:35; Hos 8:14; 13:6
[i]**32:19** Law 26:30; Za 78:59; Amo 6:8; Yer 44:21-23; Za 106:40
[j]**32:20** Kum 31:17; Za 4:6; 44:24; Kum 9:23
[k]**32:21** Hes 25:11; 1Kor 10:22; 1Fal 16:13, 26; 2Fal 17:15; Yer 8:19; Yon 2:8; Rum 10:19; Za 31:6; Yer 2:8; 10:8; 16:19
[l]**32:22** Za 7:11; Hes 16:31-35; Za 18:7-8; Yer 15:14; Mao 4:11; Amo 7:4; Law 26:20

23 [a]“Nitalundika majanga juu yao
na kutumia mishale yangu dhidi
yao.
24 [b]Nitatuma njaa kali dhidi yao
maradhi mabaya,
yateketezayo na tauni ya kufisha;
nitawapelekea meno makali ya
wanyama mwitu,
na sumu ya nyoka wale
watambaao mavumbini.
25 [c]Barabarani upanga utawakosesha
watoto;
nyumbani mwao hofu itatawala.
Vijana wao wa kiume na wa kike
wataangamia,
pia watoto wachanga na wazee
wenye mvi.
26 [d]Nilisema ningewatawanya
na kufuta kumbukumbu lao
katika mwanadamu.
27 [e]Lakini nilihofia dhihaka za adui,
adui asije akashindwa kuelewa,
na kusema, ‘Mikono yetu imeshinda;
BWANA hakufanya yote haya.’ ”

28 [f]Wao ni taifa lisilo na akili,
hakuna busara ndani yao.
29 [g]Laiti wangekuwa na hekima
wangefahamu hili,
na kutambua mwisho wao
utakuwa aje!
30 [h]Mtu mmoja angewezaje kufukuza
elfu moja,
au wawili kufukuza elfu kumi,
kama si kwamba Mwamba wao
amewauza,
kama si kwamba BWANA
amewaacha?
31 [i]Kwa kuwa mwamba wao si kama
Mwamba wetu,
sawasawa na vile adui zetu
wanavyokiri.
32 [j]Mzabibu wao unatoka kwenye
mzabibu wa Sodoma,
na kutoka kwenye mashamba ya
Gomora.
Zabibu zake zimejaa sumu,
na vishada vyake vimejaa
uchungu.
33 [k]Mvinyo wao ni sumu ya nyoka,
sumu yenye kufisha ya swila.

34 [l]“Je, hili sikuliweka akiba
na kulifungia kwenye vyumba
vyangu vya hazina?
35 [m]Ni juu yangu kulipiza kisasi;
nitalipiza.
Wakati utakapowadia, mguu wao
utateleza;
siku yao ya maafa ni karibu,
na maangamizo yao yanawajia
haraka.”

36 [n]BWANA atawahukumu watu wake,
na kuwahurumia watumishi wake
atakapoona nguvu zao zimekwisha
wala hakuna yeyote aliyebaki,
mtumwa au aliye huru.

---

[a]**32:23** Kum 29:21; 2Sam 22:15; Ay 6:4; Za 7:13; 18:14; 45:5; 77:17; 120:4; Isa 5:28; 49:2; Eze 5:16; Hab 3:9-11
[b]**32:24** Mwa 26:1; 41:55; 42:5; 2Sam 24:13; 1Nya 21:12; Kum 28:22; Za 91:6; Mwa 37:20; Ay 20:16; Za 58:4; Yer 8:17; Amo 5:18-19; Mik 7:17; Ay 20:16
[c]**32:25** Isa 24:17; Yer 14:18; Mao 1:20; Eze 7:15; 2Kor 7:5; 2Nya 36:17; Isa 13:18; Yer 4:31; Mao 2:21
[d]**32:26** Kum 4:27; Hes 14:12; Ay 18:17; Za 34:16; 37:28; 109:15; Isa 14:20
[e]**32:27** Kum 9:26-28; Za 140:8; Isa 11:13; Yer 40:2-3
[f]**32:28** Isa 1:3; 5:13; 27:11; Yer 8:7
[g]**32:29** Kum 5:29; Za 81:13; Isa 47:7; Mao 1:9
[h]**32:30** Law 26:8; Amu 2:14; 3:8; 4:2; 10:7; 1Sam 12:9; Hes 21:34; 1Sam 23:7; Za 31:18; 44:12; 106:41; Isa 50:1; 54:6
[i]**32:31** Mwa 49:24; Kut 14:25
[j]**32:32** Yer 23:14; Ay 6:4; 20:16; Kum 29:18
[k]**32:33** Za 58:4
[l]**32:34** Ay 14:17; Yer 2:22; Hos 13:12
[m]**32:35** Mwa 4:24; Yer 51:6; Mwa 30:2; Kut 32:34; Za 54:5; Rum 12:19; Ebr 10:30; Za 17:5; 35:6; 37:31; 38:16; 66:9; 73:2; 94:18; 121:3; Mit 4:19; Yer 23:12; Eze 7:8-9
[n]**32:36** Ebr 10:30; Amo 7:3; Law 26:43-45; Kum 30:1-3; Amu 2:18; Za 90:13; 102:13; 103:13; 106:45; 135:14; Yoe 2:14; 1Fal 14:10; 21:21; 2Fal 9:8

37 [a]Atasema: "Sasa iko wapi miungu
yao,
mwamba walioukimbilia,
38 [b]miungu wale waliokula mafuta ya
dhabihu zao
na kunywa mvinyo wa sadaka zao
za vinywaji?
Wainuke basi, wawasaidie!
Wawapeni basi ulinzi!

39 [c]"Tazama basi, Mimi mwenyewe,
Mimi Ndiye!
Hakuna mungu mwingine ila
Mimi.
Mimi ninaua na Mimi ninafufua,
Mimi nimejeruhi na Mimi
nitaponya,
wala hakuna awezaye kuokoa
kutoka mkononi mwangu.
40 [d]Ninainua mkono wangu kuelekea
mbinguni na kusema:
Hakika kama niishivyo milele,
41 [e]wakati ninapounoa upanga wangu
unaometameta
na mkono wangu unapoushika ili
kutoa hukumu,
nitalipiza kisasi juu ya adui zangu
na kuwalipiza wale
wanaonichukia.
42 [f]Nitailevya mishale yangu kwa
damu,
wakati upanga wangu ukitafuna
nyama:
damu ya waliochinjwa pamoja na
mateka,
vichwa vya viongozi wa adui."

43 [g]Furahini, enyi mataifa, pamoja na
watu wake,
kwa kuwa atailipiza damu ya
watumishi wake,
atalipiza kisasi juu ya adui zake
na kufanya upatanisho
kwa ajili ya nchi na watu wake.

44 [h]Mose na Yoshua[i] mwana wa Nuni
wakaja, wakanena maneno yote ya wimbo
watu wakiwa wanasikia. 45 Mose alipomaliza
kuyasoma maneno haya yote kwa Israeli
wote, 46 [j]akawaambia, "Yawekeni moyoni
maneno yote ambayo nimewatangazia kwa
makini siku hii ya leo, ili kwamba mpate
kuwaagiza watoto wenu wayatii kwa bidii
maneno yote ya sheria hii. 47 [k]Siyo maneno
matupu tu kwenu, bali ni uzima wenu. Kwa
hayo mtaishi maisha marefu katika nchi
mnayovuka Yordani kuimiliki."

*Mose Aelezwa Kuhusu Kifo Chake*

48 [l]Siku hiyo hiyo BWANA akamwambia
Mose, 49 [m]"Kwea katika mapangano ya
Mlima Abarimu hadi kilima cha Nebo
kilichoko Moabu, ng'ambo ya Yeriko,
na uitazame Kanaani, nchi ninayowapa
Waisraeli kama milki yao wenyewe.
50 [n]Utafia kwenye mlima huo unaokwea
na kukusanyika pamoja na watu wako,
kama ndugu yako Aroni alivyofia juu ya
Mlima Hori naye akakusanyika kwa watu
wake. 51 [o]Hii ni kwa sababu ninyi wawili
mlivunja uaminifu nami mbele ya Waisraeli
kwenye maji ya Meriba-Kadeshi katika
Jangwa la Sini, na kwa sababu hamkuuinua
utakatifu wangu miongoni mwa Waisraeli.

[a]**32:37** Amu 10:14; Yer 2:28; 11:12
[b]**32:38** Hes 25:1-2; Yer 11:12; 44:8; 25
[c]**32:39** Isa 41:4; 43:10; 44:7; 46:4; 48:12; 1Sam 2:6; 2Fal 5:7; Za 68:20; Yn 11:25-26; Kut 15:26; Ay 5:18; 15:11; Za 147:3; Isa 6:10; 19:22; 30:26; 53:5; 57:18; Yer 33:6; Hos 6:1; Mal 4:2; 1Pet 2:24; Ay 9:12; 10:7; Za 7:2; 50:22; Isa 43:13; Dan 4:35; Hos 5:14
[d]**32:40** Mwa 14:22; 21:23; Ufu 1:18
[e]**32:41** Amu 7:20; Za 7:12; 45:3; Isa 27:1; 34:6; 66:16; Yer 12:12; Eze 21:9-10; Za 149:7; Yer 46:10; Neh 1:2; Za 137:8; Yer 25:14; 50:29; 51:24, 56
[f]**32:42** 2Sam 2:26; Yer 12:12; 44:1; 46:10-14
[g]**32:43** Za 137:6; Isa 25:9; 65:18; 66:10; Rum 15:10; 2Fal 9:7; Ufu 6:10; Isa 1:24; Yer 9:9; Za 65:3; 79:9
[h]**32:44** Hes 13:8, 16
[i]44 Yoshua, yaani Yehoshea kwa Kiebrania, maana yake ni Yehova ni Mwokozi.
[j]**32:46** Kum 6:6; Yn 1:17; 7:19; Kum 6:7
[k]**32:47** Kum 30:20; 33:25; Kut 23:26; Isa 65:22
[l]**32:48** Hes 27:12
[m]**32:49** Hes 27:12; 32:3; 22:1; Law 14:34
[n]**32:50** Mwa 25:8; Hes 27:13; 20:22; 29
[o]**32:51** Eze 47:19; Hes 13:21; 20:11-13; 27:14

52 [a]Kwa hiyo, utaiona tu nchi kwa mbali;
wewe hutaingia nchi ninayowapa watu wa
Israeli."

*Mose Anayabariki Makabila*

33 [b]Hii ndiyo baraka Mose mtu wa Mungu
aliyotamka kwa Waisraeli kabla ya
kifo chake. 2 [c]Alisema:

"BWANA alikuja kutoka Mlima Sinai,
akachomoza kama jua juu yao
kutoka Mlima Seiri,
akaangaza kutoka Mlima Parani.
Alikuja pamoja na watakatifu
makumi elfu
kutoka kusini,
kutoka materemko ya mlima
wake.
3 [d]Hakika ni wewe ambaye huwapenda
watu,
watakatifu wako wote wamo
mkononi mwako.
Miguuni pako wote wanasujudu
na kutoka kwako wanapokea
mafundisho,
4 [e]sheria ile Mose aliyotupa sisi,
tulio milki ya kusanyiko la
Yakobo.
5 [f]Alikuwa mfalme juu ya Yeshuruni[g]
wakati viongozi wa watu
walipokusanyika,
pamoja na makabila ya Israeli.

6 [h]"Reubeni na aishi, asife,
wala watu wake wasiwe
wachache."

7 Akasema hili kuhusu Yuda:

"Ee BWANA, sikia kilio cha Yuda,
mlete kwa watu wake.
Kwa mikono yake mwenyewe
hujitetea.
Naam, uwe msaada wake
dhidi ya adui zake!"

8 [i]Kuhusu Lawi alisema:

"Thumimu yako na Urimu[j] yako
ulimpa,
mtu yule uliyemfadhili.
Ulimjaribu huko Masa
na kushindana naye
kwenye maji ya Meriba.
9 [k]Alinena hivi kuhusu baba yake na
mama yake,
'Mimi siwahitaji kamwe.'
Akawasahau jamaa zake,
asiwatambue hata watoto wake,
lakini akaliangalia neno lako
na kulilinda Agano lako.
10 [l]Humfundisha Yakobo mausia yako
na Israeli sheria yako.
Hufukiza uvumba mbele zako
na sadaka nzima za kuteketezwa
juu ya madhabahu yako.
11 [m]Ee BWANA, bariki ustadi wake
wote,
nawe upendezwe na kazi ya
mikono yake.
Vipige viuno vya wale wainukao
dhidi yake;
wapige adui zake hata wasiinuke
tena."

12 [n]Kuhusu Benyamini akasema:

---

[a]**32:52** Kum 34:1-3; 3:27
[b]**33:1** Mwa 27:4; Yos 14:6; 1Sam 2:27; 9:6; 1Fal 12:22; 13:1; 2Fal 1:9-13; 5:2; Yer 35:4
[c]**33:2** Kut 19:18; Za 68:8; Yos 11:17; Amu 5:4; Za 50:2; 80:1; 94:1; Hes 10:12; Za 89:7; Dan 4:13; 7:10; 8:13; Zek 14:5; Mdo 7:53; Gal 3:19; Ebr 2:2; Ufu 5:11
[d]**33:3** Kum 4:37; 7:6; Lk 10:39; Ufu 4:10; Hos 11:1; Kum 14:2
[e]**33:4** Kum 4:2; Yn 1:7; 7:19; Za 19:11
[f]**33:5** Kut 16:8; 1Sam 10:19; Za 10:16; 149:2; Hes 23:21; Kum 32:15; Ay 29:25
[g]5 Yeshuruni maana yake ni Yeye aliye mnyofu, yaani Israeli.
[h]**33:6** Mwa 34:5
[i]**33:8** Mwa 29:34; Kut 28:30; Za 106:16; Hes 14:22; 27:21; Kut 17:7
[j]8 Thumimu na Urimu maana yake Nuru na Kweli; vifaa hivi viliwekwa kwenye kifuko cha kifuani cha kisibau cha kuhani mkuu ili kujua mapenzi ya Mungu kwenye mambo ya kutatanisha.
[k]**33:9** Kut 32:26-29; Za 61:5; Mal 2:5
[l]**33:10** Ezr 7:10; Neh 8:18; Za 119:151; Yer 23:22; Mal 2:6; Law 10:11; Kum 17:8-11; 13:9-13; Kut 30:7; Law 16:12-13; Za 51:19
[m]**33:11** 2Sam 24:23; Za 20:3; 51:19
[n]**33:12** Mwa 35:18; Kum 4:37-38; 12:10; 32:8; Kut 19:4; Za 60:5; 127:2; Kut 28:12

"Mwache mpenzi wa BWANA
apumzike salama kwake,
kwa maana humkinga mchana
kutwa,
na yule BWANA ampendaye
hupumzika kati ya mabega yake."

13 [a]Kuhusu Yosefu akasema:

"BWANA na aibariki nchi yake
kwa umande wa thamani
kutoka mbinguni juu,
na vilindi vya maji
vilivyotulia chini;
14 pamoja na vitu vilivyo bora sana
viletwavyo na jua,
na vitu vizuri sana vinavyoweza
kutolewa na mwezi;
15 [b]pamoja na zawadi bora sana
za milima ya zamani
na kwa wingi wa baraka
za vilima vya milele;
16 [c]pamoja na baraka nzuri mno
za ardhi na ukamilifu wake,
na upendeleo wake yeye
aliyeishi kwenye kichaka
kilichokuwa kinawaka moto.
Hivi vyote na vikae juu ya kichwa
cha Yosefu,
juu ya paji la uso la aliye mkuu
miongoni mwa ndugu zake.
17 [d]Katika fahari yeye ni kama fahali
mzaliwa wa kwanza;
pembe zake ni pembe za nyati,
na kwa pembe hizo atapiga mataifa,
hata yaliyo miisho ya dunia.
Hivyo ndivyo yalivyo makumi elfu
ya Efraimu;
hivyo ndivyo yalivyo maelfu ya
Manase."

18 [e]Kuhusu Zabuloni akasema:

"Shangilia, Zabuloni, wakati wa
kutoka nje,
nawe Isakari, katika mahema
yako.
19 [f]Watawaita mataifa kwenye mlima,
na huko mtatoa dhabihu za haki;
watajifurahisha kwa wingi uliojaza
bahari,
kwa hazina zilizofichwa
mchangani."

20 [g]Kuhusu Gadi akasema:

"Atabarikiwa yeye aongezaye milki
ya Gadi!
Gadi huishi huko kama simba,
akirarua kwenye mkono au
kichwa.
21 [h]Alijichagulia nchi nzuri kuliko zote
kwa ajili yake mwenyewe;
fungu la kiongozi lilikuwa
limehifadhiwa
kwa ajili yake.
Viongozi wa watu walipokusanyika,
alitimiza haki ya mapenzi ya
BWANA,
na hukumu zake kuhusu Israeli."

22 [i]Kuhusu Dani akasema:

"Dani ni mwana simba,
akiruka kutoka Bashani."

23 [j]Kuhusu Naftali akasema:

"Naftali amejaa tele upendeleo wa
BWANA,
naye amejaa baraka yake;
atarithi magharibi na kusini."

24 [k]Kuhusu Asheri akasema:

---

[a]**33:13** Mwa 30:24; 27:28; Za 148:7; Mwa 49:25
[b]**33:15** Hab 3:6
[c]**33:16** Kut 3:2; Mwa 37:8
[d]**33:17** 1Sam 2:10; 2Sam 22:3; Eze 34:21; Hes 23:22; 1Fal 22:11; Za 44:5; Mwa 41:51-52
[e]**33:18** Mwa 30:18-20; 49:13-15
[f]**33:19** Kut 15:17; Za 48:1; Isa 2:3; 65:11; 66:20; Yer 31:6; Za 4:5; 51:19; Isa 18:7; 23:18; 45:14; 60:5; 11; 61:6; Hag 2:7; Zek 14:14
[g]**33:20** Mwa 30:11; Kum 3:12-17; Mwa 49:19
[h]**33:21** Hes 32:1-5, 31-32; 34:14; Yos 22:1-3; 4:14
[i]**33:22** Yos 19:47; Amu 18:27
[j]**33:23** Mwa 30:8; Yos 19:32
[k]**33:24** Mwa 30:13; 49:20; Kum 32:13; Ay 29:6

"Aliyebarikiwa zaidi sana katika
wana ni Asheri;
yeye na apate upendeleo kwa
ndugu zake,
yeye na anawe miguu yake
kwenye mafuta.
25 [a]Makomeo ya malango yako yawe
chuma na shaba,
nazo nguvu zako zitakuwa sawa
na siku zako.

26 [b]"Hakuna mwingine kama Mungu wa
Yeshuruni,
ambaye hupanda juu ya mbingu ili
akusaidie,
na juu ya mawingu katika utukufu
wake.
27 [c]Mungu wa milele ni kimbilio lako,
na chini kuna mikono ya milele.
Atamfukuza adui yako mbele yako,
akisema, 'Mwangamize yeye!'
28 [d]Hivyo Israeli ataishi salama peke
yake.
Mzao wa Yakobo ni salama
katika nchi ya nafaka na divai mpya,
mahali ambapo mbingu
hudondosha umande.
29 [e]Ee Israeli, wewe umebarikiwa!
Ni nani kama wewe,
taifa lililookolewa na BWANA?
Yeye ni ngao yako na msaada wako,
na upanga wako uliotukuka.
Adui zako watatetemeka mbele
yako,
nawe utapakanyaga
mahali pao pa juu."[f]

*Kifo Cha Mose*

34 [g]Kisha Mose akaupanda mlima Nebo
kutoka tambarare za Moabu mpaka
kilele cha Pisga, ng'ambo ya Yeriko. Huko
BWANA akamwonyesha nchi yote: kutoka
Gileadi mpaka Dani, 2 [h]Naftali yote, nchi
ya Efraimu na Manase, nchi yote ya Yuda
mpaka bahari ya magharibi,[i] 3 [j]Negebu
na nchi yote kuanzia Bonde la Yeriko,
Mji wa Mitende, hadi Soari. 4 [k]Kisha
BWANA akamwambia, "Hii ndiyo nchi
niliyomwahidi Abrahamu na Isaki na
Yakobo kwa kiapo niliposema, 'Nitawapa
wazao wako.' Nimekuruhusu uione kwa
macho yako, lakini hutavuka kuingia."
5 [l]Naye Mose mtumishi wa BWANA akafa
huko Moabu, kama BWANA alivyokuwa
amesema. 6 [m]Mungu akamzika huko Moabu,
katika bonde mkabala na Beth-Peori, lakini
hakuna ajuaye kaburi lake lilipo mpaka leo.
7 [n]Mose alikuwa na umri wa miaka mia moja
na ishirini alipofariki; hata hivyo nguvu ya
macho yake haikufifia wala mwili wake
haukudhoofika. 8 [o]Waisraeli wakaomboleza
kwa ajili ya Mose kwenye tambarare za
Moabu kwa siku thelathini, mpaka wakati
wa kulia na kuomboleza ulipopita.

---

[a]**33:25** Neh 3:3; 7:3; Za 147:13; Kum 32:47
[b]**33:26** Kum 32:15; Za 18:10; 68:33; Kum 10:14; Za 104:3; 2Sam 22:10; Za 18:9; 68:4; Dan 7:13; Kut 15:7
[c]**33:27** Kut 15:18; Isa 40:28; 57:15; Za 9:9; 84:1; 90:1; 91:9; Mwa 21:33; Kut 34:11; Yos 24:18; Kum 7:2
[d]**33:28** Kut 33:16; Law 25:18; Kum 32:8; Za 16:9; Mit 1:33; Isa 14:30; Mwa 27:28
[e]**33:29** Za 1:1; 132:1-2; 144:15; 118:7; 18:44; 66:3; 54:4; 81:15; 10:14; 18:1; 27:1; 9; 30:10; 70:5; 115:9-11; 2Sam 22:45; Kum 4:7; 32:13; Mwa 15:1; Kut 18:4; Hab 3:19; Hos 13:9; Isa 45:24; 2Sam 7:23; Hes 33:52

[f]29 Utapakanyaga mahali pao pa juu maana yake mtakanyaga juu ya miili yao.
[g]**34:1** Hes 32:3; 21:10; Kum 32:49, 52; Yos 19:40-48; Amu 18:28
[h]**34:2** Kut 23:31; Kum 11:24; Hes 34:6; Yos 15:12
[i]2 Yaani Bahari ya Mediterania.
[j]**34:3** Mwa 12:9; 13:10; Amu 1:16; 3:13; 2Nya 28:15
[k]**34:4** Mwa 28:13; 12:7; Yos 21:43; Kum 3:23, 27
[l]**34:5** Hos 12:7; Yos 1:1-2; Mwa 25:8
[m]**34:6** Kum 3:29; Yud 9
[n]**34:7** Kut 7:7; Yos 14:10; Mwa 27:1; 15:15; Kum 31:2
[o]**34:8** Hes 21:11; 20:29; Mwa 37:34; 50:3; 10; 50:3; 2Sam 11:27; 1Sam 25:1; Isa 57:1; Mdo 8:2

9 [a]Basi Yoshua mwana wa Nuni alijazwa
roho ya hekima kwa sababu Mose alikuwa
ameweka mikono yake juu yake. Kwa hiyo
Waisraeli wakamsikiliza na wakafanya yale
ambayo BWANA alikuwa amemwagiza
Mose.
10 [b]Tangu wakati huo, katika Israeli
hajainuka nabii mwingine kama Mose,
ambaye BWANA alimjua uso kwa uso,
11 [c]aliyetenda ishara zote zile za miujiza
na maajabu ambayo BWANA alimtuma
kuyatenda huko Misri, yaani kwa Farao
na maafisa wake wote na nchi yake yote.
12 [d]Kwa kuwa hakuna mtu yeyote aliyewahi
kuonyesha nguvu nyingi ama kutenda
matendo ya kutisha ambayo Mose aliwahi
kuyafanya mbele ya Israeli yote.

---

[a]**34:9** Mwa 41:38; Kut 28:3; 31:3; Isa 11:2; 1Fal 9:12; Kum 31:14; Mdo 6:6; Dan 6:3; Kum 27:18; Hes 11:17; 27:18

[b]**34:10** Mwa 20:7; Kum 18:15-18; 5:4; Kut 33:11; Hes 12:6-8

[c]**34:11** Kum 4:34; 7:19; Kut 11:3

[d]**34:12** Ebr 3:1-6; Kum 4:34

# YOSHUA

*BWANA Anamwagiza Yoshua*

1 [a]Baada ya kifo cha Mose mtumishi wa
BWANA, BWANA akamwambia Yoshua
mwana wa Nuni, msaidizi wa Mose:
2 [b]“Mtumishi wangu Mose amekufa. Sasa
basi, wewe pamoja na watu wote hawa,
jiandaeni kuvuka huu Mto Yordani kuingia
nchi ambayo karibu nitawapa wana wa
Israeli. 3 [c]Kila mahali nyayo za miguu
yenu zitakapokanyaga nimewapa, kama
vile nilivyomwahidi Mose. 4 [d]Nchi yenu
itaenea kuanzia jangwa hili hadi Lebanoni,
tena kuanzia mto mkubwa wa Frati, yaani
nchi yote ya Wahiti, hadi Bahari ile Kubwa[e]
iliyoko upande wa magharibi. 5 [f]Hakuna
mtu yeyote atakayeweza kushindana na
wewe siku zote za maisha yako. Kama
vile nilivyokuwa pamoja na Mose, ndivyo
nitakavyokuwa pamoja na wewe, sitakuacha
wala sitakupungukia.

6 [g]“Uwe hodari na shujaa, kwa sababu
wewe ndiwe utakayewaongoza watu
hawa kuirithi nchi niliyowaapia baba zao
kuwapa. 7 [h]Uwe hodari na uwe na ushujaa
mwingi. Uwe na bidii kutii sheria yote
aliyokupa Mose mtumishi wangu, usiiache
kwa kugeuka kuelekea kuume au kushoto,
ili upate kufanikiwa popote uendako.
8 [i]Usiache Kitabu hiki cha Sheria kiondoke
kinywani mwako; yatafakari maneno
yake usiku na mchana, ili upate kuwa
mwangalifu kufanya kila kitu sawasawa
na yote yaliyoandikwa ndani yake. Ndipo
utakapofanikiwa na kisha utastawi. 9 [j]Je,
si mimi niliyekuamuru? Uwe hodari na
shujaa. Usihofu wala usivunjike moyo,
kwa kuwa BWANA Mungu wako atakuwa
pamoja nawe kokote uendako.”

10 [k]Ndipo Yoshua akawaagiza maafisa wa
watu akisema, 11 [l]“Pitieni katika kambi yote
mkawaambie watu, ‘Wekeni tayari mahitaji
yenu. Siku tatu kuanzia sasa mtavuka
hii Yordani ili kuingia na kuimiliki nchi
ambayo BWANA Mungu wenu anawapa iwe
yenu wenyewe.’ ”

12 [m]Lakini kwa Wareubeni, Wagadi na
nusu ya kabila la Manase, Yoshua akasema,
13 [n]“Kumbukeni agizo lile Mose mtumishi
wa BWANA alilowapa: ‘BWANA Mungu
wenu anawapa ninyi raha, naye amewapa
nchi hii.’ 14 [o]Wake zenu, watoto wenu na
mifugo yenu watakaa katika nchi ile Mose
aliyowapa mashariki ya Yordani, lakini
mashujaa wenu wote, wakiwa wamevikwa
silaha kikamilifu lazima wavuke mbele ya
ndugu zenu. Imewapasa kuwasaidia ndugu
zenu hadi 15 [p]BWANA awape nao raha, kama
alivyokwisha kufanya kwa ajili yenu hadi
wao pia watakapokuwa wamemiliki nchi
ile BWANA Mungu wenu anayowapa. Baada

---

[a]**1:1** Kut 14:31; Kum 34:5; Ufu 15:3; Kut 17:9; 24:13; Hes 32:20; Yos 22:2-4
[b]**1:2** Hes 13:29; 35:10; Mwa 15:14; 12:7; Kum 1:24-25
[c]**1:3** Kum 11:24; Mwa 50:24; Hes 13:2; Kum 1:8
[d]**1:4** Kum 3:25; Mwa 2:14; 10:15; 23:10; Kut 3:8; Hes 34:2-12; Ezr 4:20
[e]4 Yaani Bahari ya Mediterania.
[f]**1:5** Kum 7:24; Mwa 26:3; 39:2; Amu 6:12; 1Sam 10:7; Yer 1:8; 30:11; Mwa 28:1; Kum 4:31
[g]**1:6** 2Sam 2:7; 1Fal 2:2; Isa 41:6; Yoe 3:9-10; Kum 1:21; 31:6; Amu 5:21; Yer 3:18; 7:7
[h]**1:7** Kum 29:9; 1Fal 2:3; 3:3; Ezr 7:26; Za 78:10; 119:136; Isa 42:24; Yer 26:4-6; 32:23; 44:10; Hes 12:7; Ay 42:7; Kum 5:32; Yos 23:6; Kum 4:2; 5:33; 11:8; Yos 11:15
[i]**1:8** Kum 28:61; Za 147:19; Kut 4:15; Isa 59:21; Mwa 24:63; Kum 29:9; 1Sam 18:14; Isa 52:13; 53:10; Yer 23:5
[j]**1:9** Kum 31:6; Yos 10:8; 2Fal 19:6; Isa 34:5; 37:6; Kum 1:21; Ay 4:5; Kum 31:8; Yer 1:8
[k]**1:10** Kum 1:15
[l]**1:11** Yos 3:2; 1Sam 17:22; Isa 10:28; Mwa 40:13; Hes 35:10; 33:53
[m]**1:12** Hes 32:33
[n]**1:13** Kut 33:14; Za 55:6; Isa 11:10; 28:12; 30:15; 32:18; 40:31; Yer 6:16; 45:3
[o]**1:14** Kum 3:19; Hes 32:26; Kut 13:18; Yos 4:12
[p]**1:15** Hes 32:20-22; Yos 22:1-4

ya hilo, mwaweza kurudi na kukalia nchi
yenu wenyewe, ambayo Mose mtumishi wa
Bwana aliwapa mashariki mwa Yordani
kuelekea linakochomoza jua.”
16 [a]Ndipo wakamjibu Yoshua, “Chochote
ambacho umetuagiza tutafanya na popote
utakapotutuma tutakwenda. 17 [b]Kama
vile tulivyomtii Mose kikamilifu, ndivyo
tutakavyokutii wewe. Bwana Mungu wako
na awe pamoja nawe tu kama vile alivyokuwa
pamoja na Mose. 18 Yeyote atakayeasi neno
lako na kuacha kuyatii maneno yako, au
chochote utakachowaamuru, atauawa. Uwe
imara na hodari tu!”

*Rahabu Na Wapelelezi*

2 [c]Kisha Yoshua mwana wa Nuni kwa siri
akawatuma wapelelezi wawili kutoka
Shitimu, akawaambia, “Nendeni mkaikague
hiyo nchi, hasa Yeriko.” Kwa hiyo wakaenda
na kuingia kwenye nyumba ya kahaba
mmoja jina lake Rahabu na kukaa humo.
2 [d]Mfalme wa Yeriko akaambiwa,
“Tazama! Baadhi ya Waisraeli wamekuja
huku usiku huu kuipeleleza nchi.” 3 [e]Hivyo
mfalme wa Yeriko akatuma huu ujumbe
kwa Rahabu: “Watoe wale watu waliokujia
na kuingia nyumbani mwako, kwa sababu
wamekuja kuipeleleza nchi yote.”
4 [f]Lakini huyo mwanamke alikuwa
amewachukua hao watu wawili na
kuwaficha. Akasema, “Naam, watu hao
walikuja kwangu, lakini sikujua walikotoka.
5 [g]Kulipoingia giza, wakati wa kufunga
lango la mji, watu hao waliondoka. Sijui
njia waliyoiendea. Wafuatilieni haraka.
Huenda mkawapata.” 6 [h](Lakini alikuwa
amewapandisha darini akawafunika kwa
mabua ya kitani aliyokuwa ameyatandika
darini.) 7 [i]Basi hao watu wakaondoka
kuwafuatilia hao wapelelezi katika njia
ile inayoelekea vivuko vya Yordani, mara
tu wafuatiliaji walipotoka nje, lango
likafungwa.
8 [j]Kabla wale wapelelezi hawajalala,
Rahabu akawaendea huko juu darini,
9 [k]akawaambia, “Ninajua kuwa Bwana
amewapa nchi hii na hofu kuu imetuangukia
kwa sababu yenu, kiasi kwamba wote
waishio katika nchi hii wanayeyuka kwa
hofu kwa sababu yenu. 10 [l]Tumesikia jinsi
Bwana alivyokausha maji ya Bahari ya
Shamu kwa ajili yenu mlipotoka Misri,
pia lile mlilowatendea Sihoni na Ogu,
wafalme wawili wa Waamori mashariki
mwa Yordani, ambao mliwaangamiza
kabisa. 11 [m]Tuliposikia juu ya hili, mioyo
yetu iliyeyuka na kila mmoja alikosa ujasiri
kwa sababu yenu, kwa maana Bwana
Mungu wenu ni Mungu juu mbinguni
na duniani chini. 12 [n]Sasa basi, tafadhali
niapieni kwa Bwana, kwamba mtaitendea
hisani jamaa ya baba yangu, kwa kuwa
mimi nimewatendea hisani. Nipeni ishara
ya uaminifu 13 [o]kwamba mtayahifadhi
maisha ya baba yangu na mama yangu,
ndugu zangu wa kiume na wa kike, pamoja
na wale wote walio wa kwao na kwamba
mtatuokoa na kifo.”

[a]**1:16** Hes 27:20; 32:25
[b]**1:17** Hes 32:25; Kum 1:21; 31:6; Mwa 21:22; 26:24, 28; 1Sam 16:18; 20:13; 1Fal 1:37; Za 20:1-4, 9; Rum 8:31
[c]**2:1** Mwa 42:9; Hes 25:1; Yos 3:1; Yoe 3:18; Hes 21:32; Amu 18:2; Hes 33:48; Yos 6:17, 25; Ebr 11:31
[d]**2:2** Za 127:1; Mit 21:30
[e]**2:3** Yos 6:23
[f]**2:4** Yos 6:22; 6:17; 2Sam 17:19-20; 2Fal 6:19
[g]**2:5** Amu 5:8; 9:35; 16:2; Ebr 11:31
[h]**2:6** Amu 15:14; Mit 31:13; Isa 19:9; Kut 1:19; Yos 6:25; 2Sam 17:19; Yak 2:25; Kut 1:17
[i]**2:7** Hes 22:1; Amu 3:28; 7:24; 12:5-6; Isa 16:2
[j]**2:8** Kum 22:8; Amu 16:27; 2Sam 16:22; Neh 8:16; Isa 15:3; 22:1; Yer 32:29
[k]**2:9** Mwa 35:5; Kut 15:14-15; Mwa 35:5; Kum 2:25; 11:25
[l]**2:10** Mwa 8:1; Kut 14:21; Yos 3:17; Za 74:15; Hes 23:22; 21:21; Mwa 10:16; 14:7; Yos 9:10
[m]**2:11** Mwa 42:28; Kum 2:25; Za 107:26; Yon 1:5; Kut 15:14; Yos 5:1; 7:5; 2Sam 4:1; Za 22; 14; Isa 13:7; 19:1; Yer 51:30; Nah 2:10; 2Fal 5:15; 19:15; Dan 6:26; Mwa 14:19; Hes 20:14; Kum 4:39
[n]**2:12** Mwa 24:8; 47:31; 24; 12; Rut 3:10; Mwa 24:14; Kut 3:12; Yos 4:6; 1Sam 2:34; 2Fal 19:29
[o]**2:13** Yos 6:23

14 [a]Wale watu wakamhakikishia Rahabu,
“Uhai wetu kwa uhai wenu! Ikiwa hutatoa
habari ya nini tunachofanya, wakati BWANA
atakapotupa nchi hii, tutawatendea kwa
hisani na kwa uaminifu.”
15 [b]Kisha akawateremsha dirishani kwa
kamba, kwa kuwa nyumba yake aliyokuwa
anaishi ilikuwa sehemu ya ukuta wa mji.
16 [c]Alikuwa amewaambia, “Nendeni vilimani
ili wale wafuatiliaji wasiwapate. Jificheni
huko kwa siku tatu mpaka watakaporudi,
hatimaye mwende zenu.”
17 [d]Wale watu wakamwambia, “Hiki
kiapo ulichotuapisha hakitatufunga,
18 [e]isipokuwa, hapo tutakapoingia katika
nchi hii, utakuwa umefunga hii kamba
nyekundu dirishani pale ulipotuteremshia
na kama utakuwa umewaleta baba yako
na mama yako, ndugu zako na jamaa yako
yote ndani ya nyumba yako. 19 [f]Ikiwa mtu
yeyote atatoka nje ya nyumba yako akaenda
mtaani, damu yake itakuwa juu ya kichwa
chake mwenyewe, hatutawajibika. Lakini
yule ambaye atakuwa ndani pamoja nawe,
kama mkono wa mtu yeyote ukiwa juu yake
damu yake itakuwa juu ya vichwa vyetu.
20 [g]Lakini ikiwa utatoa habari ya shughuli
yetu tunayofanya, tutakuwa tumefunguliwa
kutoka kwenye kiapo hiki ulichotufanya
tuape.”
21 Naye akajibu, “Nimekubali. Na iwe
kama mnavyosema.” Kwa hiyo akaagana
nao, nao wakaondoka. Yeye akaifunga ile
kamba nyekundu dirishani.
22 Walipoondoka, wakaelekea vilimani na
kukaa huko siku tatu, hadi wale waliokuwa
wakiwafuatilia wakawa wamewatafuta njia
nzima na kurudi pasipo kuwapata. 23 Ndipo
wale watu wawili wakaanza kurudi.
Wakashuka kutoka kule vilimani, wakavuka
mto na kuja kwa Yoshua mwana wa Nuni,
na kumweleza kila kitu kilichowapata.
24 [h]Wakamwambia Yoshua, “Hakika BWANA
ametupa nchi yote mikononi mwetu; watu
wote wanayeyuka kwa hofu kwa sababu
yetu.”

*Kuvuka Yordani*

3 [i]Yoshua na Waisraeli wote wakaondoka
asubuhi na mapema kutoka Shitimu,
wakaenda mpaka Mto Yordani, ambako
walipiga kambi kabla ya kuvuka. 2 [j]Baada
ya siku tatu maafisa wakapita katika
kambi yote, 3 [k]wakitoa maagizo kwa watu,
wakiwaambia: “Mtakapoona Sanduku
la Agano la BWANA Mungu wenu,
likichukuliwa na Walawi ambao ndio
makuhani, mtaondoka hapo mlipo na
kulifuata. 4 [l]Ndipo mtakapotambua njia
mtakayoiendea, kwa kuwa hamjawahi
kuipita kabla. Lakini msisogee karibu, bali
kuwe na umbali wa dhiraa 2,000[m] kati yenu
na Sanduku.”
5 [n]Ndipo Yoshua akawaambia hao watu,
“Jitakaseni, kwa kuwa kesho BWANA
atatenda mambo ya kushangaza katikati
yenu.”
6 [o]Yoshua akawaambia makuhani,
“Liinueni Sanduku la Agano mkatangulie
mbele ya watu.” Hivyo wakaliinua na
kutangulia mbele yao.
7 [p]Ndipo BWANA akamwambia Yoshua,
“Leo nitaanza kukutukuza machoni pa
Israeli yote, ili wapate kujua kuwa niko
pamoja nawe kama nilivyokuwa pamoja na

---

[a]**2:14** 1Fal 20:39-42; 2Fal 10:24; Mwa 47:29; Mt 5:7; Amu 1:24; Mt 5:7
[b]**2:15** Yer 38:6, 11; Mwa 26:8; Amu 5:28; 1Sam 19:12; Mdo 9:25; Ebr 11:31
[c]**2:16** Yak 2:25; Mwa 14:10; Ebr 11:31
[d]**2:17** Mwa 24:8; Kut 20:7
[e]**2:18** Yos 6:23; Mwa 7:1; 19:12, 17; Es 8:6; Mdo 11:14; 2Tim 1:16
[f]**2:19** Law 20:9; Eze 33:4; Hes 34:26, 27
[g]**2:20** Mwa 24:8; 47:31
[h]**2:24** Yos 10:8; 11:6; Amu 3:28; 7:9; 20:28; 1Sam 14:10; Kut 15:15
[i]**3:1** Yos 2:1; Mwa 13:10; Ay 40:23; Hes 25:1; 33:49
[j]**3:2** Mwa 40:13; Yos 2:16; Kum 1:16; Yos 1:11
[k]**3:3** Hes 10:33; 4:15; Kum 31:9; 1Fal 8:3; 1Sam 6:15
[l]**3:4** Hes 35:5; Kut 19:12; Kum 28:58; 1Nya 16:30; Za 2:11; 96:9; Ebr 12:28
[m]4 Dhiraa 2,000 ni sawa na mita 900.
[n]**3:5** Kut 20:1; Law 11:44; Amu 6:13; 1Nya 16:9, 24; Za 26:7; 75:1; Kut 10:10; Hes 11:18; Yos 7:13; 1Sam 16:5; Yos 2:16
[o]**3:6** Hes 4:15
[p]**3:7** Yos 4:14; 1Nya 29:25; Yos 1:5

Mose. 8 Uwaambie makuhani wanaochukua
Sanduku la Agano, 'Mnapofika kwenye
ukingo wa maji ya Yordani, nendeni
mkasimame ndani ya mto.' "
9 Yoshua akawaambia Waisraeli, "Njooni
hapa msikilize maneno ya BWANA Mungu
wenu. 10 [a]Hivi ndivyo mtakavyojua ya
kuwa Mungu aliye hai yupo katikati yenu,
na kwamba kwa hakika atawafukuza
mbele yenu hao Wakanaani, Wahiti,
Wahivi, Waperizi, Wagirgashi, Waamori na
Wayebusi. 11 [b]Tazameni, Sanduku la Agano
la BWANA wa dunia yote litaingia ndani ya
Mto Yordani likiwa limewatangulia. 12 [c]Sasa
basi, chagueni watu kumi na wawili kutoka
makabila ya Israeli, mtu mmoja kutoka
kila kabila. 13 [d]Mara tu nyayo za makuhani
walichukualo Sanduku la BWANA, Bwana
wa dunia yote, zitakapokanyaga ndani
ya Mto Yordani, maji hayo yatiririkayo
kutoka juu yatatindika na kusimama kama
chuguu."
14 [e]Basi, watu walipovunja kambi
ili kuvuka Yordani, makuhani
wakiwa wamebeba Sanduku la Agano
waliwatangulia. 15 [f]Wakati huu ulikuwa
wakati wa mavuno, nao Mto Yordani
ulikuwa umefurika hadi kwenye kingo
zake. Ilikuwa kawaida ya Yordani kufurika
nyakati zote za mavuno. Mara tu makuhani
wale waliokuwa wamebeba Sanduku la
Agano walipofika mtoni na nyayo zao
kuzama ndani ya yale maji, 16 [g]maji hayo
yaliyotiririka kutoka upande wa juu yaliacha
kutiririka yakasimama kama chuguu mbali
kabisa nao, kwenye mji ulioitwa Adamu
kwenye eneo la Sarethani, wakati yale maji
yaliyokuwa yanatiririka kuingia kwenye
Bahari ya Araba (yaani Bahari ya Chumvi),
yalitindika kabisa. Hivyo watu wakavuka
kukabili Yeriko.
17 [h]Wale makuhani waliobeba Sanduku
la Agano la BWANA, wakasimama imara
mahali pakavu katikati ya Mto Yordani,
wakati Waisraeli wote wakiwa wanapita
hadi taifa lote likaisha kuvuka mahali
pakavu.

### *Ukumbusho Wa Kuvuka Mto Yordani*

4 [i]Wakati taifa lote lilipokwisha kuvuka
Mto Yordani, BWANA akamwambia
Yoshua, 2 [j]"Chagua watu kumi na wawili
miongoni mwa watu, kila kabila mtu mmoja,
3 nawe uwaambie wachukue mawe kumi na
mawili katikati ya Mto Yordani, palepale
makuhani waliposimama, wayachukue na
kuyaweka mahali mtakapokaa usiku huu
wa leo."
4 [k]Basi Yoshua akawaita watu kumi na
wawili ambao alikuwa amewachagua
kutoka miongoni mwa Waisraeli, mtu
mmoja kutoka kila kabila, 5 [l]naye
akawaambia, "Mtangulie mbele ya Sanduku
la BWANA Mungu wenu, mwende katikati
ya Mto Yordani. Kila mmoja wenu atainua
jiwe begani mwake, kufuatana na hesabu ya
makabila ya Waisraeli, 6 [m]kuwa kama ishara
katikati yenu. Siku zijazo, wakati watoto
wenu watakapowauliza, 'Ni nini maana ya
mawe haya?' 7 [n]waambieni kwamba maji
ya Mto Yordani yaliyokuwa yakitiririka
yalitindika mbele ya Sanduku la Agano la
BWANA. Wakati lilipovuka Yordani, maji ya
Yordani yalitindika. Mawe haya yatakuwa
kumbukumbu kwa watu wa Israeli milele."

---

[a]**3:10** Kum 5:26; 1Sam 17:26, 36; 2Fal 19:4, 16; Za 18:46; 42:2; Isa 37:4, 17; Yer 10:10; 23:36; Dan 6:26; Hos 1:10; Mt 16:16; Kum 7:21; Mwa 26:24; Yos 17:15; 24:11; Amu 1:4; 3:5; Kut 3:8; 23:23; Kum 7:1; 9:1; 11:3; Amu 19:11; 1Nya 11:4
[b]**3:11** Kut 19:5; Kum 14:10; Ay 9:10; 28:24; 41:11; Za 50:12; 97:5; Zek 6:5; Kum 9:3
[c]**3:12** Yos 4:2-4
[d]**3:13** Yos 4:7; Kut 14:22; Isa 11:15; Za 78:13
[e]**3:14** Za 132:8; Mdo 7:44-45; Kut 25:10; 26:30; Hes 10:3; 2Nya 6:41; Ebr 9:4
[f]**3:15** 2Fal 3:6; Yos 4:18; 1Nya 12:15; Isa 8:7; Mwa 8:22; Yer 12:5; 49:19
[g]**3:16** Za 66:6; 74:15; 114:3; Ay 38:37; Za 33:7; 1Fal 4:12; 7:46; Mwa 14:3; 8:1; Kut 14:22; 2Fal 2:4
[h]**3:17** Yos 4:3-9; Kut 14:22; Yos 2:10
[i]**4:1** Kum 27:2; Yos 2:17
[j]**4:2** Yos 3:17; Hes 13:1; 34:18; Yos 1:4-15; 1Fal 18:31
[k]**4:4** Yos 3:12
[l]**4:5** Yos 3:17
[m]**4:6** Yos 2:12; Kut 10:2; 12:26; 13:14; Kum 6:20; Za 78:3-6; Isa 38:16
[n]**4:7** Yos 3:13; Kut 28:12; 12:14

8 [a]Hivyo Waisraeli wakafanya kama
Yoshua alivyowaagiza. Wakachukua mawe
kumi na mawili kutoka katikati ya Mto
Yordani, kulingana na hesabu ya kabila za
Waisraeli kama BWANA alivyomwambia
Yoshua, nao wakayabeba hadi kambini
mwao, mahali walipoyatua chini. 9 [b]Yoshua
akayasimamisha yale mawe kumi na mawili
ambayo yalikuwa katikati ya Mto Yordani,
mahali pale ambapo miguu ya makuhani
waliobeba Sanduku la Agano iliposimama.
Nayo yako huko mpaka leo.

10 Makuhani waliobeba lile Sanduku
walibakia wakiwa wamesimama katikati
ya Mto Yordani mpaka kila kitu BWANA
alichomwamuru Yoshua kilipokuwa
kimefanywa na watu, sawasawa na
vile Mose alivyokuwa amemwamuru
Yoshua. Watu wakafanya haraka kuvuka,
11 na mara tu watu wote walipokwisha
kuvuka, Sanduku la BWANA na makuhani
wakavuka watu wakiwa wanatazama.
12 [c]Wareubeni, Wagadi na nusu ya kabila
la Manase wakavuka mbele ya Waisraeli,
wakiwa wamevaa silaha, kama Mose
alivyowaamuru. 13 [d]Kiasi cha watu 40,000
waliojiandaa kwa vita walivuka mbele za
BWANA hadi nchi tambarare za Yeriko kwa
ajili ya vita.

14 [e]Siku ile BWANA akamtukuza Yoshua
mbele ya Israeli yote, nao wakamheshimu
siku zote za maisha yake, kama vile
walivyomheshimu Mose.

15 Basi BWANA akamwambia Yoshua,
16 [f]"Waamuru hao makuhani wanaolibeba
Sanduku la Ushuhuda, wapande kutoka
ndani ya Mto Yordani."

17 Kwa hiyo Yoshua akawaamuru hao
makuhani akisema, "Pandeni kutoka ndani
ya Mto Yordani."

18 [g]Nao makuhani wakapanda kutoka
ndani ya Mto Yordani wakilibeba hilo
Sanduku la Agano la BWANA. Mara tu
walipoiweka miguu yao penye kingo, nje
ya mto, maji ya Yordani yakarudi kufurika
kama ilivyokuwa kabla.

19 [h]Siku ya kumi ya mwezi wa kwanza watu
walipanda kutoka Yordani na kupiga kambi
huko Gilgali, kwenye mpaka wa mashariki
ya Yeriko. 20 Naye Yoshua akayasimamisha
huko Gilgali yale mawe kumi na mawili
ambayo walikuwa wameyachukua katikati
ya Mto Yordani. 21 Akawaambia Waisraeli,
"Wazao wenu watakapowauliza baba zao
siku zijazo wakisema, 'Mawe haya maana
yake ni nini?' 22 [i]Basi waambieni, 'Israeli
ilivukia mahali pakavu katika Mto Yordani.'
23 [j]Kwa maana BWANA Mungu wenu
alikausha maji ya Yordani mbele yenu,
hadi mlipomaliza kuvuka. BWANA Mungu
wenu alifanya haya kwa Mto Yordani
sawasawa na kile alichoifanyia Bahari ya
Shamu wakati alipoikausha mbele yetu
hadi tulipomaliza kuvuka. 24 [k]Alifanya hivi
ili kwamba mataifa yote ya dunia yapate
kujua kuwa mkono wa BWANA ni wenye
nguvu, na ili kwamba kila wakati mpate
kumcha BWANA Mungu wenu."

5 [l]Basi wafalme wote wa Waamori
magharibi ya Yordani na wafalme wote
wa Kanaani waliokuwa kwenye pwani
waliposikia jinsi BWANA alivyoukausha
Mto Yordani mbele ya Waisraeli hata
tulipokwisha kuvuka, mioyo yao ikayeyuka
kwa hofu, wala hawakuwa na ujasiri
kuwakabili Waisraeli.

*Tohara Huko Gilgali*

2 [m]Wakati huo BWANA akamwambia

---

[a]**4:8** Kut 28:21; Yos 3:17
[b]**4:9** Mwa 28:18; Yos 24:26; 1Sam 7:12; Mwa 35:20
[c]**4:12** Mwa 29:32; 30:11; 41:51; Hes 32:27-29
[d]**4:13** Kut 13:18; Hes 32:17
[e]**4:14** Yos 3:7; 1Sam 2:30; 2Nya 32:23; 1Nya 29:12
[f]**4:16** Kut 25:22; Ufu 11:19; Yos 3:15
[g]**4:18** Kut 14:27; Yos 3:15
[h]**4:19** Kum 11:30; Yos 5:9; 15:17; 1Sam 11:14-15; Amo 4:4; 5:5; Mik 6:5
[i]**4:22** Kut 14:22; Yos 3:17
[j]**4:23** Kut 14:19-22; Neh 9:11; Za 77:16-19; Isa 43:16; 63:12
[k]**4:24** 1Fal 8:60; 18:36; 2Fal 5:15; Za 67:2; 83:18; 106:8; Isa 37:20; 52:10; Kut 15:16; 1Nya 29:12; Za 44:3; 89:13; 98:1; 118:15-16; Kut 14:31
[l]**5:1** Kut 4:25; Hes 13:29; Mwa 42:28; Yos 2:9-11; Kut 15:14; Za 48:6; Eze 21:7; 1Fal 10:5
[m]**5:2** Kut 4:25; Mwa 17:10-14

Yoshua, “Tengeneza visu vya mawe
magumu sana na uwatahiri Waisraeli tena.”
3 Kwa hiyo Yoshua akatengeneza visu vya
mawe magumu sana na kutahiri Waisraeli
huko Gibeath-Haaralothi.[a]

4 [b]Hii ndiyo sababu ya Yoshua kufanya
hivyo: Wanaume wote waliotoka Misri,
wote wenye umri wa kwenda vitani,
walikufa jangwani wakiwa njiani baada
ya kuondoka Misri. 5 Watu wote waliotoka
Misri walikuwa wametahiriwa, lakini watu
wote waliozaliwa jangwani wakiwa safarini
toka Misri walikuwa hawajatahiriwa.
6 [c]Waisraeli walitembea jangwani miaka
arobaini mpaka wanaume wote wale
waliokuwa na umri wa kwenda vitani
wakati waliondoka Misri walipokwisha
kufa, kwa kuwa hawakumtii BWANA.
Kwa maana BWANA alikuwa amewaapia
kuwa wasingeweza kuona nchi ambayo
alikuwa amewaahidi baba zao katika kuapa
kutupatia, nchi inayotiririka maziwa na
asali. 7 [d]Kwa hiyo akawainua wana wao
baada yao na hawa ndio hao ambao Yoshua
aliwatahiri. Walikuwa hawajatahiriwa bado
kwa sababu walikuwa safarini. 8 [e]Baada ya
taifa lote kutahiriwa, waliendelea kukaa
kambini mpaka walipokuwa wamepona.

9 [f]BWANA akamwambia Yoshua, “Leo
nimeiondoa aibu ya Wamisri kutoka
kwenu.” Basi mahali pale pakaitwa Gilgali
hadi leo.

10 [g]Jioni ya siku ya kumi na nne ya
mwezi, wakiwa kambini huko Gilgali
katika tambarare za Yeriko, Waisraeli
wakaadhimisha Pasaka. 11 [h]Siku iliyofuata
Pasaka, katika siku ile ile, wakala mazao ya
nchi, mikate isiyotiwa chachu na nafaka za
kukaanga. 12 [i]Mana ilikoma siku iliyofuata
baada ya Waisraeli kula chakula kilichotoka
katika nchi; hapakuwa na mana tena kwa
ajili ya Waisraeli, ila mwaka huo walikula
mazao ya nchi ya Kanaani.

### *Jemadari Wa Jeshi La BWANA*

13 [j]Basi wakati Yoshua alipokuwa karibu
na Yeriko, akainua macho, akaona mtu
aliyesimama mbele yake, akiwa na upanga
mkononi uliofutwa kwenye ala. Yoshua
akamwendea na kumuuliza, “Je, wewe uko
upande wetu au upande wa adui zetu?”

14 [k]Akajibu, “La, siko upande wowote,
lakini mimi nimekuja nikiwa jemadari
wa jeshi la BWANA.” Yoshua akaanguka
kifudifudi hadi chini, akasujudu,
akamuuliza, “Je, Bwana, una ujumbe gani
kwa mtumishi wako?” 15 [l]Jemadari wa
jeshi la BWANA akajibu, “Vua viatu vyako,
kwa maana mahali hapa unaposimama ni
patakatifu.” Naye Yoshua akafanya hivyo.

### *Yeriko Yatekwa Na Kuangamizwa*

6 [m]Basi malango ya Yeriko yalifungwa kwa
uthabiti kwa ajili ya Waisraeli. Hakuna
mtu yeyote aliyetoka au kuingia.

2 [n]Kisha BWANA akamwambia Yoshua,
“Tazama, nimeitia Yeriko mikononi mwako,
pamoja na mfalme wake na watu wake
wa vita. 3 Zunguka mji mara moja pamoja
na watu wote wenye silaha. Fanya hivi
kwa siku sita. 4 [o]Uwe na makuhani saba
wakibeba mabaragumu ya pembe za kondoo
dume mbele ya Sanduku. Siku ya saba,
mzunguke mji mara saba, nao makuhani
wakipiga baragumu hizo. 5 [p]Utakapowasikia

[a]3 Gibeath-Haaralothi maana yake ni Kilima cha Magovi.
[b]**5:4** Hes 1:3; Kum 2:14, 16; Hes 14:29; 26:64
[c]**5:6** Hes 32:13; Yos 14:10; Za 107:4; Kut 16:35; Hes 14:23-35; Kum 2:14; Kut 3:8
[d]**5:7** Hes 14:31
[e]**5:8** Mwa 34:25
[f]**5:9** Kum 11:30; 1Sam 14:6; Law 18:3; Yos 24:14; Eze 20:7
[g]**5:10** Kut 12:6; 12:11
[h]**5:11** Hes 15:19; Kut 12:15; Law 23:14; Hes 9:5
[i]**5:12** Kut 16:35
[j]**5:13** Mwa 18:2; Hes 22:23; Mwa 32:24; Kut 23:23; Mdo 1:10; Zek 1:8
[k]**5:14** Mwa 17:3; 19:1; Dan 10:13; Ufu 2:17; Law 9:24; Hes 16:22
[l]**5:15** Mwa 28:17; Kut 3:5; Mdo 7:33; Kut 19:10-13; Za 22:3; 29:2; Isa 6:3; 1Nya 26:25-29; 1Sam 2:2
[m]**6:1** Yos 24:11
[n]**6:2** Kum 7:24; Yos 8:1; Amu 11:21; 2Sam 5:19; Neh 9:24; Dan 5:18-19
[o]**6:4** Kut 19:13; Law 25:9; Hes 10:8; Amu 7:16
[p]**6:5** Kut 19:13; 1Sam 6:15; Ezr 3:11; 10:12; Za 42:4; 95:1; Isa 8:9; 42:13

wamepaliza sauti kubwa ya baragumu,
watu wote wapige kelele kwa sauti kuu,
kisha ukuta wa mji utaanguka na watu
watapanda, kila mtu akiendelea mbele.”
6 Ndipo Yoshua mwana wa Nuni akaita
makuhani na kuwaambia, “Chukueni
Sanduku la Agano la BWANA na makuhani
saba wachukue baragumu za pembe
za kondoo dume mbele yake.” 7 [a]Naye
akawaagiza watu, “Songeni mbele!
Mkauzunguke mji, na walinzi wenye silaha
watangulie mbele ya Sanduku la BWANA.”
8 [b]Baada ya Yoshua kuzungumza na
watu, wale makuhani saba wenye kuzibeba
zile baragumu saba mbele za BWANA,
wakatangulia mbele, wakipiga baragumu
zao na Sanduku la Agano la BWANA
likawafuata. 9 [c]Walinzi waliokuwa na
silaha wakaenda mbele ya hao makuhani
waliopiga hizo baragumu na hao walinzi
wa nyuma wakafuata Sanduku. Wakati
wote huu baragumu zilikuwa zikipigwa.
10 [d]Bali Yoshua alikuwa amewaagiza watu,
“Msipige kelele ya vita, msipaze sauti
zenu, wala kusema neno lolote mpaka
siku ile nitakayowaambia mpige kelele.
Ndipo mtapiga kelele!” 11 Basi akalipeleka
Sanduku la BWANA kuzungushwa huo mji,
likizungushwa mara moja. Kisha watu
wakarudi kambini kulala.
12 [e]Yoshua akaamka mapema asubuhi
iliyofuata nao makuhani wakalichukua
Sanduku la BWANA. 13 [f]Wale Makuhani
saba wakizibeba zile baragumu saba
wakatangulia mbele ya Sanduku la
BWANA wakizipiga. Watu wenye silaha
wakatangulia mbele yao na walinzi wa
nyuma wakalifuata Sanduku la BWANA,
huku baragumu hizo zikiendelea kulia.
14 Siku ya pili wakauzunguka mji mara
moja na kurudi kambini. Wakafanya hivi
kwa siku sita.
15 [g]Siku ya saba, wakaamka asubuhi
na mapema wakauzunguka mji kama
walivyokuwa wakifanya, isipokuwa
siku ile waliuzunguka mji mara saba.
16 [h]Walipouzunguka mara ya saba, makuhani
walipopiga baragumu kwa sauti kubwa,
Yoshua akawaamuru watu akisema, “Pigeni
kelele! Kwa maana BWANA amewapa mji
huu! 17 [i]Mji huu pamoja na vyote vilivyomo
ndani yake utawekwa wakfu kwa BWANA.
Ila Rahabu tu, yule kahaba na wote ambao
wako pamoja naye nyumbani mwake
ndio watakaosalimishwa, kwa sababu
aliwaficha wale wapelelezi tuliowatuma.
18 [j]Lakini mjiepushe na vitu vilivyowekwa
wakfu, msije mkachukua chochote katika
hivyo, msije mkajiletea maangamizi katika
maskani ya Israeli na kuiletea taabu.
19 [k]Fedha yote na dhahabu, vyombo vya
shaba na chuma ni vitakatifu kwa BWANA,
lazima viletwe katika hazina yake.”
20 [l]Wakati baragumu zilipopigwa, watu
walipiga kelele, na katika sauti ya baragumu,
na watu kupaza sauti, ukuta ukaanguka;
hivyo kila mtu akapanda akiendelea mbele
na kuuteka mji. 21 [m]Wakauweka mji wakfu
kwa BWANA, na kila chenye uhai ndani yake
walikiangamiza kwa upanga, wanaume kwa
wanawake, vijana kwa wazee, ng’ombe,
kondoo na punda.
22 [n]Yoshua akawaambia wale watu wawili
waliokuwa wameipeleleza nchi, “Nendeni
nyumbani kwa yule kahaba, mleteni
pamoja na wote waliomo nyumbani mwake,

[a]**6:7** Kut 14:15; Hes 10:35; 1Sam 4:3; 7:1
[b]**6:8** Yos 4:13
[c]**6:9** Hes 2:31; Isa 52:12, 13; Hes 10:25; Isa 42:11-13
[d]**6:10** 1Sam 4:5; Ezr 3:11
[e]**6:12** Kum 31:25
[f]**6:13** 1Nya 15:26; Gal 6:9
[g]**6:15** 1Fal 18:44; 2Fal 4:35; 5:14
[h]**6:16** Amu 7:20; 2Nya 14:14
[i]**6:17** Law 27:28; Kum 20:17; Isa 13:5; 24:1; 34:2-5; Mal 4:6; Yos 2:14; Mwa 13:3; 1Sam 15:6; Mt 10:41; 25:40; Ebr 6:10; 11:31; Yak 2:25
[j]**6:18** Yos 7:1, 12, 25, 26; 1Nya 2:7; Kum 7:26; 13:17; Isa 52:11; Rum 12:9; 2Kor 6:17; Efe 5:11; 1The 5:2; 1Fal 18:17, 18
[k]**6:19** Hes 31:22
[l]**6:20** Law 25:9; Amu 6:34; 7:22; 1Fal 1:41; Isa 18:3; Yer 4:21; 42:14; Amo 2:2; Ebr 11:30
[m]**6:21** Kum 20:16; 1Sam 15:3, 8; 1Fal 20:42; Yer 48:18; Ufu 18:21
[n]**6:22** Mwa 42:9; Yos 2:4; Hes 21:32; Yos 2:14; Ebr 11:30-31

kulingana na kiapo chenu kwake.” 23 [a]Basi
wale vijana waliofanya upelelezi wakaenda
kumleta Rahabu, baba yake na mama yake,
na ndugu zake na watu wote waliokuwa
pamoja naye. Wakaleta jamaa yake yote na
kuwaweka mahali nje ya kambi ya Israeli.
24 [b]Kisha wakauchoma mji wote na kila
kitu kilichokuwamo ndani yake. Lakini
fedha, dhahabu, vyombo vya shaba na
vya chuma wakaviweka katika hazina
ya nyumba ya BWANA. 25 [c]Lakini Yoshua
akamhifadhi Rahabu yule kahaba, jamaa
yake yote na wote waliokuwa wa kwake,
kwa sababu aliwaficha watu waliotumwa
na Yoshua kuipeleleza Yeriko, naye anaishi
miongoni mwa Waisraeli hata leo.
26 [d]Wakati ule Yoshua akatamka kiapo
hiki akasema, “Aliyelaaniwa mbele za
BWANA ni mtu atakayeinuka kuujenga tena
mji huu wa Yeriko:

“Kwa gharama ya mzaliwa wake wa
kwanza wa kiume
ataiweka misingi yake;
kwa gharama ya mtoto wake wa
mwisho
atayaweka malango yake.”

27 [e]Hivyo BWANA alikuwa pamoja na
Yoshua, na sifa zake zikaenea katika nchi
yote.

*Dhambi Ya Akani*

7 [f]Lakini Waisraeli hawakuwa waaminifu
kuhusu vile vitu vilivyowekwa wakfu;
Akani mwana wa Karmi, mwana wa
Zabdi, mwana wa Zera, wa kabila la Yuda,
alivichukua baadhi ya hivyo vitu. Hasira ya
BWANA ikawaka dhidi ya Israeli.
2 [g]Basi Yoshua akatuma watu kutoka
Yeriko waende Ai, karibu na Beth-Aveni
mashariki ya Betheli, akawaambia,
“Pandeni mkaipeleleze nchi.” Basi wale
watu wakapanda wakaipeleleza Ai.
3 Waliporudi kwa Yoshua, wakasema,
“Si lazima watu wote waende kupigana
na Ai. Watume watu elfu mbili au tatu
wakauteke huo mji. Usiwachoshe watu
wote, kwa sababu huko kuna watu
wachache tu.” 4 [h]Basi wakapanda kama
watu elfu tatu tu, lakini wakashambuliwa
na watu wa Ai, 5 [i]ambao waliwaua watu
kama thelathini na sita miongoni mwao.
Wakawafukuza Waisraeli kutoka lango la
mji hadi Shebarimu, nao wakawauwa huko
kwenye materemko. Kutokana na hili mioyo
ya watu ikayeyuka ikawa kama maji.
6 [j]Ndipo Yoshua akayararua mavazi yake,
akaanguka kifudifudi mbele ya Sanduku
la BWANA, na akabakia hapo mpaka
jioni. Wazee wa Israeli nao wakafanya
vivyo hivyo wakatia mavumbi vichwani
mwao. 7 [k]Yoshua akasema, “Ee BWANA
Mwenyezi, kwa nini umewavusha watu
hawa ng’ambo ya Yordani ili kututia
mikononi mwa Waamori watuangamize?
Laiti tungeliridhika kukaa ng’ambo ile
nyingine ya Yordani! 8 Ee BWANA, niseme
nini sasa, ikiwa sasa Israeli ameshafukuzwa
na adui zake? 9 [l]Wakanaani na watu
wengine wa nchi watasikia habari hii, nao
watatuzunguka na kutufutilia jina letu
duniani. Utafanya nini basi kwa ajili ya
jina lako mwenyewe lililo kuu?”

[a]**6:23** Yos 2:13
[b]**6:24** Hes 31:10; Kum 13:16
[c]**6:25** Amu 1:25; Yos 2:1; 2:1, 6; Ebr 11:31
[d]**6:26** 1Sam 14:24; Hes 5:21; 1Fal 16:34
[e]**6:27** Mwa 39:2; Hes 14:43; Yos 9:1; 1Nya 14:17; Amu 1:9; 2Sam 7:9; Rum 8:31; 1Sam 2:30
[f]**7:1** Yos 6:18; 1Nya 2:7; Yos 22:20; Hes 1:4; Kut 4:14; 32:20; Law 10:6
[g]**7:2** Mwa 12:8; Yos 8:1, 28; 18:12; 1Sam 14:23; Hos 4:15; 5:8; 10:5; Mwa 12:8; Yos 12:16; 16:1; Amu 1:22; 1Sam 30:27; 2Fal 23:15; Yer 48:13; Amo 3:14; 4:4; 5:5-6; 7:10, 13; Hes 21:32
[h]**7:4** Law 26:17; Kum 28:25; 32:30; Isa 30:17; 59:2
[i]**7:5** Yos 22:20; Mwa 42:28; Za 22; 14; Isa 13:7; Eze 21:7; Nah 2:10; Law 26:36
[j]**7:6** Mwa 37:29; 17:3; 1Nya 21:16; Eze 9:8; Amu 20:23; Yos 8:10; 9:11; 20:4; 23:2; 1Sam 4:12; 2Sam 13:19; 15:32; Neh 9:1; Ay 2:12; Eze 27:30; Ufu 18:19
[k]**7:7** 1Sam 4:3; Kut 5:22; Hes 14:16; 2Fal 3:10
[l]**7:9** Kut 32:12; Kum 9:28; 28:58; 1Sam 12:22; Za 48:10; 106:8; Yer 14:21

10 Bwana akamwambia Yoshua,
“Simama! Unafanya nini hapo chini
kifudifudi? 11 [a]Israeli ametenda dhambi.
Wamekiuka agano langu nililowaamuru
kulishika. Wamechukua baadhi ya vitu
vilivyowekwa wakfu, wameiba, wamesema
uongo, wameviweka pamoja na mali zao.
12 [b]Ndiyo sababu Waisraeli hawawezi
kusimama dhidi ya adui zao. Wanawapa
visogo na kukimbia kwa kuwa wanastahili
maangamizi. Sitakuwa pamoja nanyi tena
mpaka mwangamize kila kitu miongoni
mwenu kilichotengwa kwa maangamizi.

13 [c]“Nenda, ukawatakase watu. Waambie,
‘Jitakaseni mjiandae kwa kesho; kwa
sababu hili ndilo asemalo Bwana, Mungu
wa Israeli: Kitu kilichowekwa wakfu kipo
katikati yenu, ee Israeli. Hamwezi kusimama
dhidi ya adui zenu mpaka mtakapokiondoa.

14 [d]“ ‘Asubuhi, mjihudhurishe kabila kwa
kabila. Itakuwa kabila lile atakalolitwaa
Bwana litakuja mbele ukoo kwa ukoo,
ukoo ule atakaoutwaa Bwana utakuja
mbele jamaa kwa jamaa, nayo jamaa ile
atakayoitwaa Bwana itakuja mbele mtu
kwa mtu. 15 [e]Yule atakayekutwa na vitu
vilivyowekwa wakfu, atateketezwa kwa
moto, pamoja na vitu vyote alivyo navyo.
Kwa kuwa amelivunja agano la Bwana na
kufanya kitu cha aibu katika Israeli!’ ”

16 Kesho yake asubuhi na mapema Yoshua
akawaamuru Israeli kuja mbele kabila kwa
kabila; na Yuda akatwaliwa. 17 [f]Koo za Yuda
zikaja mbele, naye akawatwaa Wazera.
Akaamuru ukoo wa Wazera kuja mbele
jamaa kwa jamaa, nayo jamaa ya Zabdi
ikatwaliwa. 18 [g]Yoshua akaamuru watu wa
jamaa ya Zabdi kuja mbele mtu kwa mtu,
naye Akani mwana wa Karmi, mwana wa
Zabdi, mwana wa Zera, wa kabila la Yuda,
akatwaliwa.

19 [h]Ndipo Yoshua akamwambia Akani,
“Mwanangu, mtukuze Bwana, Mungu wa
Israeli, nawe ukiri kwake. Niambie ni nini
ulichotenda; usinifiche.”

20 Akani akamjibu Yoshua, “Ni kweli!
Nimetenda dhambi dhidi ya Bwana,
Mungu wa Israeli. Hili ndilo nililofanya:
21 [i]Nilipoona katika nyara joho zuri la
kutoka Babeli, shekeli mia mbili[j] za fedha,
na kabari ya dhahabu ya uzito wa shekeli
hamsini,[k] nikavitamani na nikavichukua.
Tazama, vimefichwa ardhini ndani ya hema
langu, pamoja na hiyo fedha chini yake.”

22 Kwa hiyo Yoshua akatuma wajumbe,
nao wakapiga mbio mpaka hemani, tazama,
vile vitu vilikuwa vimefichwa hemani
mwake, pamoja na ile fedha chini yake.
23 Wakavichukua vile vitu toka mle hemani,
wakamletea Yoshua pamoja na Waisraeli
wote, na wakavitandaza mbele za Bwana.

24 [l]Basi Yoshua, pamoja na Israeli yote,
wakamchukua Akani mwana wa Zera,
pamoja na ile fedha, lile joho, ile kabari ya
dhahabu, wanawe na binti zake, ng’ombe,
punda na kondoo wake, hema yake pamoja
na vitu vyote alivyokuwa navyo, wakavileta
katika Bonde la Akori. 25 [m]Yoshua akasema,
“Kwa nini umeleta taabu hii juu yetu?
Bwana ataleta taabu juu yako leo hii.”

Ndipo Israeli yote ikampiga Akani kwa
mawe, na baada ya kuwapiga jamaa yake
yote kwa mawe, wakawateketeza kwa

---

[a]**7:11** Kut 9:27; Kum 29:27; Yos 24:16-27; 2Fal 17:7; Hos 10:9; Yos 6:17-19; 23:16; Amu 2:20; 1Sam 15:24; Za 78:10; Mdo 5:1-2

[b]**7:12** Law 26:37; Za 18:40; 21:12; Law 26:17; Yos 6:18; Za 44:9; 60:10

[c]**7:13** Law 11:44; Yos 3:5; Kut 19:10

[d]**7:14** 1Sam 10:19; Mit 16:33; 1Sam 14:41-42; Yn 1:7; Mdo 1:24-26

[e]**7:15** Yos 6:18; Kum 7:25; 2Fal 25:9; 1Nya 14:12; Isa 37:19; Yer 43:12; Eze 30:16; 1Sam 14:39; Mwa 34:7

[f]**7:17** Hes 26:20

[g]**7:18** Yos 7:1; Law 24:11; Yn 1:7; Mdo 5:1-10; Yer 2:26; Mit 13:21; Hes 32:23; Mwa 4:7

[h]**7:19** Kut 14:17; 1Sam 6:5; Za 96:8; Isa 42:12; Yer 13:16; Yn 9:24; Law 5:5; 1Sam 14:43

[i]**7:21** Mwa 34:29; 49:27; Kum 7:25; Efe 5:5; 1Tim 6:10; Kut 20:17; 1Fal 21:1; 2Fal 5:20-27; Mit 15:27; Hab 2:9; Lk 12:15; Rum 7:7, 8

[j]21 Shekeli 200 za fedha ni sawa na kilo 2.3.

[k]21 Shekeli 50 ni sawa na gramu 600.

[l]**7:24** Hes 16:27; Yos 7:26; 15:7; Isa 65:10; Hos 2:15

[m]**7:25** Yos 6:18; Law 20:2; Kum 17:5; 1Fal 12:18; 2Nya 10:18; 24:21; Neh 9:26; Mwa 38:24; 1Nya 2:7; Gal 5:12

moto. 26 [a]Wakakusanya lundo la mawe juu ya Akani, ambalo lipo mpaka leo. Naye BWANA akageuka kutoka hasira yake kali. Kwa hiyo mahali pale pakaitwa Bonde la Akori[b] tangu siku hiyo.

### *Mji Wa Ai Waangamizwa*

8 [c]Ndipo BWANA akamwambia Yoshua, "Usiogope, wala usivunjike moyo. Chukua jeshi lote la vita uende pamoja nalo kuishambulia Ai. Kwa kuwa nimeshamweka mikononi mwako mfalme wa Ai, pamoja na watu wake, mji wake na nchi yake. 2 [d]Utafanya Ai na mfalme wake kama ulivyofanya kwa mji wa Yeriko na mfalme wake, isipokuwa mnaweza kuchukua mateka wake na mifugo wake, kwa ajili yenu. Weka waviziaji upande wa nyuma ya mji."

3 Basi Yoshua na jeshi lote wakainuka kushambulia Ai. Akachagua watu mashujaa elfu thelathini walio bora miongoni mwa wapiganaji wake, akawapeleka wakati wa usiku 4 [e]akiwaagiza: "Sikilizeni kwa makini. Mtavizia nyuma ya mji. Msiende mbali sana na mji. Wote kuweni macho. 5 [f]Mimi na watu walio pamoja nami, tutaukabili mji, kisha itakuwa hapo watu watakapotoka nje kupigana nasi, kama walivyofanya hapo kwanza, sisi tutawakimbia. 6 Watatufuatilia mpaka tutakapokuwa tumewavuta mbali na mji kwa kuwa watasema, 'Wanatukimbia, kama walivyofanya hapo awali.' Hivyo tutakapowakimbia, 7 [g]ninyi inawapasa mwinuke mtoke huko mafichoni na kuuteka mji. BWANA Mungu wenu atautia mkononi mwenu. 8 [h]Mtakapokuwa mmeuteka mji, uteketezeni kwa moto. Fanyeni kama vile BWANA alivyoamuru. Angalieni, nimewaagiza."

9 [i]Ndipo Yoshua akawatuma watu, nao wakaenda mahali pa kujificha, wakawa wanavizia kati ya Betheli na Ai, kuelekea upande wa magharibi wa Ai, lakini Yoshua akalala miongoni mwa watu usiku huo.

10 [j]Asubuhi na mapema siku iliyofuatia, Yoshua akawakutanisha watu wake, na yeye na viongozi wa Israeli wakawa mbele ya watu kwenda Ai. 11 Watu wote wa vita waliokuwa pamoja naye walipanda, wakakaribia na kufika mbele ya mji. Wakapiga kambi kaskazini mwa Ai, pakiwa na bonde kati yao na huo mji. 12 [k]Yoshua alikuwa amewachukua watu wapatao elfu tano, akawaweka katika uavizi kati ya Betheli na Ai, upande wa magharibi wa mji. 13 Wakawaweka askari katika maeneo yao: wale wote waliokuwa kambini wakawa kaskazini ya mji na wale waliokuwa wakivizia wakawa upande wa magharibi. Usiku huo Yoshua akaenda katika lile bonde.

14 [l]Mfalme wa Ai alipoona jambo hili, yeye pamoja na watu wote wa mji wakatoka kwa haraka asubuhi na mapema, ili kukutana na Israeli katika vita mahali fulani panapotazamana na Araba. Lakini hakujua kwamba kulikuwa kumewekwa waviziaji dhidi yake nyuma ya mji. 15 [m]Yoshua na Israeli wote wakaruhusu kurudishwa nyuma mbele yao, na kuelekea jangwani. 16 [n]Watu wote wa Ai wakaitwa ili kuwafuatia, nao wakavutwa kumfuatia Yoshua mbali na mji. 17 Hakuna hata mwanaume mmoja aliyebakia Ai wala Betheli ambaye hakufuatia Israeli. Wakauacha mji wazi na kuwafuatia Israeli.

18 [o]Ndipo BWANA akamwambia Yoshua,

---

[a]**7:26** 2Sam 18:17; Mwa 35:20; Hes 25:4; Kum 13:17; Isa 65:10; Hos 2:15; Yos 8:29; 2Sam 18:17; Mao 3:53; Kum 13:17; 2Sam 21:14
[b]26 Akori yamaanisha taabu
[c]**8:1** Mwa 26:24; Kum 31:6; Hes 14:9; Kum 1:21; Yos 10:7; 7:2; 9:3; 10:1; 12:9; 6:2
[d]**8:2** Mwa 49:27; Kum 20:14; Amu 9:43; 20:29; Yos 6:21
[e]**8:4** Amu 20:29; 2Nya 13:13
[f]**8:5** Amu 20:35
[g]**8:7** Amu 7:7; 1Sam 23:4
[h]**8:8** Amu 20:29-38; 2Sam 13:28; Yos 1:16
[i]**8:9** 2Nya 13:13
[j]**8:10** Mwa 22:3; Yos 7:6; 6:12; Za 101:8; 119:60; Mhu 9:10; Yer 21:12
[k]**8:12** Mwa 12:8; 28:19
[l]**8:14** Kum 1:1; Amu 20:34; Mt 24:39; 1The 5:1-3; 2Pet 2:3
[m]**8:15** Amu 20:36; Yos 15:61; 18:12
[n]**8:16** Amu 20:31; Kut 14:3-4; Za 9:16
[o]**8:18** Ay 41:26; Za 35:3; Kut 4:2; 17:9-12; 14:16; Kum 7:23-24; 9:3; Yos 1:5; Yer 49:3

“Inua huo mkuki ulio mkononi mwako
kuuelekeza Ai, kwa kuwa nitautia huo
mji mkononi mwako.” Hivyo Yoshua
akauelekeza mkuki wake Ai. 19 [a]Mara tu
alipofanya hivi, wale watu waliokuwa
mavizioni wakaondoka upesi kutoka mahali
pao na kukimbilia mbele. Wakaingia ndani
ya mji, wakauteka na kuutia moto kwa
haraka.

20 [b]Watu wa Ai wakaangalia nyuma,
wakauona moshi wa huo mji ukielekea
angani lakini hawakuwa na nafasi ya
kutoroka kwa upande wowote, kwa kuwa
wale Waisraeli waliokuwa wanawakimbia
kuelekea jangwani walikuwa wamegeuka
nyuma kuwakabili wakimbizaji wao.
21 Basi Yoshua na Israeli wote walipoona
kwamba waviziaji wameshauteka mji
na moshi ulikuwa unapaa juu kutoka
kwenye mji, wakawageukia watu wa Ai na
kuwashambulia. 22 [c]Wale waviziaji nao pia
wakatoka nje ya mji dhidi yao, hivi kwamba
wakashikiwa katikati, Waisraeli wakiwa
pande zote mbili. Israeli wakawaua, bila
kuwaachia yeyote aliyenusurika wala
aliyetoroka. 23 [d]Lakini wakamchukua
mfalme wa Ai akiwa hai na kumleta kwa
Yoshua.

24 Israeli ilipomaliza kuwaua wanaume
wote wa Ai katika mashamba na jangwani
walipokuwa wamewafukuzia, na baada
ya kila mmoja wao kuuawa kwa upanga,
Waisraeli wote wakarudi Ai na kuwaua
wale waliokuwa wamebakia mjini. 25 [e]Watu
kumi na mbili elfu, waume kwa wake,
waliangamia siku ile, yaani watu wote wa
Ai. 26 [f]Kwa maana Yoshua hakuurudisha ule
mkono wake uliokuwa umeuinua mkuki hadi
alipomaliza kuwaangamiza wote walioishi
Ai. 27 [g]Lakini Israeli wakajichukulia mifugo
na nyara za mji huu, kama vile Bwana
alivyokuwa amemwagiza Yoshua.

28 [h]Kwa hiyo Yoshua akauchoma moto mji
wa Ai na kuufanya kuwa lundo la magofu
la kudumu, mahali pa ukiwa hadi leo.
29 [i]Akamwangika mfalme wa Ai kwenye mti
na kumwacha hapo mpaka jioni. Wakati
wa jua kutua, Yoshua akawaamuru wautoe
mwili wake kwenye mti na kuutupa kwenye
ingilio la lango la mji. Kisha wakalundika
mawe makubwa mengi juu yake, ambayo
yamesalia mpaka leo.

### *Agano Linafanywa Upya Katika Mlima Ebali*

30 [j]Kisha Yoshua akajenga madhabahu ya
Bwana, Mungu wa Israeli, katika Mlima wa
Ebali, 31 [k]kama Mose mtumishi wa Bwana
alivyokuwa amewaamuru Waisraeli.
Akaijenga sawasawa na ilivyoandikwa katika
Kitabu cha Sheria ya Mose: madhabahu ya
mawe yasiyochongwa, ambayo juu yake
hakuna chombo cha chuma kilichotumika.
Hapo juu yake wakamtolea Bwana sadaka
za kuteketezwa na kutoa sadaka za amani.[l]
32 [m]Pale, mbele ya Waisraeli Yoshua
akanakili juu ya hayo mawe sheria ya Mose,
aliyokuwa ameiandika. 33 [n]Israeli yote,
wageni na wazawa sawasawa, wakiwa na
wazee wao, maafisa na waamuzi, walikuwa
wamesimama pande zote mbili za Sanduku
la Agano la Bwana, wakiwaelekea wale
waliokuwa wamelichukua, yaani makuhani,
ambao ni Walawi. Nusu ya watu ilisimama
mbele ya Mlima Gerizimu na nusu hiyo
ingine ikasimama mbele ya Mlima Ebali,
kama vile Mose mtumishi wa Bwana
alivyokuwa ameamuru hapo mwanzo
alipotoa maagizo ya kuwabariki watu wa
Israeli.

[a]**8:19** Amu 20:33
[b]**8:20** Amu 20:40
[c]**8:22** Kum 7:2; Yos 10:1; Law 27:29; Ay 20:5; Lk 17:26-30
[d]**8:23** 1Sam 15:8
[e]**8:25** Kum 20:16-18
[f]**8:26** Hes 21:2; 17:12
[g]**8:27** Hes 31:22, 26; Mt 20:15
[h]**8:28** Hes 31:10; Yos 7:2; Yer 49:3; Kum 13:16; Yos 10:1; Mwa 35:20; 2Fal 19:25; Isa 17:1; 25:2; Yer 9:11
[i]**8:29** Kum 21:23; Yn 19:31; 2Sam 18:17; Yos 10:26, 27; Za 107:40; 110:5; Yos 7:26; 10:27
[j]**8:30** Kum 11:29; Kut 20:24; Mwa 8:20; 12:7-8
[k]**8:31** Kut 20:24-25; Kum 27:6-7
[l]31 Sadaka za ushirika
[m]**8:32** Kum 27:8
[n]**8:33** Law 16:29; Kum 31:12; 11:29; Yn 4:20; 1Nya 15:11-13; Law 24:22; Hes 15:16

34 [a]Hatimaye, Yoshua akasoma maneno
yote ya sheria, yaani baraka na laana,
kama vile ilivyoandikwa katika Kitabu
cha Sheria. 35 [b]Hakuna neno lolote katika
yale yote ambayo Mose alikuwa ameamuru
ambalo Yoshua hakulisomea kusanyiko lote
la Israeli, ikiwa ni pamoja na wanawake
na watoto, na wageni walioishi miongoni
mwao.

*Udanganyifu Wa Wagibeoni*

9 [c]Basi ikawa wafalme wote waliokuwa
magharibi mwa Yordani waliposikia
juu ya haya yote, wale waliokuwa katika
nchi ya vilima, upande wa magharibi mwa
vilima na katika pwani yote ya hiyo Bahari
Kuu,[d] hadi kufikia Lebanoni (wafalme wa
Wahiti, Waamori, Wakanaani, Waperizi,
Wahivi na Wayebusi), 2 [ef]wakajiunga
pamoja ili kupigana vita dhidi ya Yoshua
na Israeli.
3 [g]Hata hivyo, watu wa Gibeoni
waliposikia juu ya hayo yote Yoshua
aliyowatendea watu wa Yeriko na Ai, 4 nao
wakaamua kufanya hila: Wakajifanya kama
wajumbe wakiwa na punda waliobebeshwa
mizigo wakiwa na magunia yaliyochakaa
na viriba vya mvinyo vikuukuu vyenye
nyufa zilizozibwa. 5 Walivaa miguuni
mwao viatu vilivyoraruka na kushonwa
kisha wakavaa nguo kuukuu. Chakula chao
kilikuwa mkate uliokauka na kuingia koga.
6 [h]Ndipo wakamwendea Yoshua kambini
huko Gilgali wakamwambia yeye pamoja
na watu wa Israeli, "Tumetoka katika nchi
ya mbali, fanyeni mkataba nasi."
7 [i]Basi watu wa Israeli wakawaambia hao
Wahivi, "Lakini huenda mnakaa karibu
nasi, twawezaje basi kufanya mapatano
nanyi?"
8 [j]Wakamwambia Yoshua, "Sisi ni
watumishi wako."
Yoshua akawauliza, "Ninyi ni nani, nanyi
mnatoka wapi?"
9 [k]Nao wakamjibu: "Watumishi wako
wametoka nchi ya mbali sana kwa ajili
ya umaarufu wa BWANA Mungu wenu.
Kwa kuwa tumesikia taarifa zake: hayo
yote aliyofanya huko Misri, 10 [l]pia yale
yote aliyowatendea wafalme wawili wa
Waamori mashariki ya Yordani; huyo
Sihoni mfalme wa Heshboni na Ogu mfalme
wa Bashani, aliyetawala huko Ashtarothi.
11 Basi wazee wetu na wale wote wanaoishi
katika nchi yetu walituambia, 'Chukueni
chakula cha safari; nendeni mkakutane na
watu hao na kuwaambia, "Sisi tu watumishi
wenu, fanyeni mapatano nasi." ' 12 Mkate
huu wetu ulikuwa wa moto tulipoufunga
siku tulipoanza safari kuja kwenu, lakini
sasa angalia jinsi ulivyokauka na kuota
ukungu. 13 Viriba hivi vya mvinyo vilikuwa
vipya tulipovijaza, lakini ona jinsi vilivyo
na nyufa. Nguo zetu na viatu vimechakaa
kwa ajili ya safari ndefu."
14 [m]Basi watu wa Israeli wakavikagua
vyakula vyao bila kupata shauri kutoka
kwa BWANA. 15 [n]Ndipo Yoshua akafanya
mapatano ya amani pamoja nao kuwaacha
waishi, nao viongozi wa kusanyiko
wakathibitisha kwa kiapo.
16 Siku ya tatu baada ya hao kufanya
mapatano na Wagibeoni, Waisraeli
wakapata habari kuwa hao watu ni jirani zao
waliokuwa wanaishi karibu nao. 17 [o]Ndipo

[a]**8:34** Kum 28:61; 31:11; Neh 8:3; Kum 29:20-21
[b]**8:35** Kut 12:38; Kum 31:12; Yos 1:8
[c]**9:1** Hes 13:17; 34:6; Kum 3:25; Mwa 13:7; Yos 3:10; 11:19; Kut 3:17
[d]1 Yaani Bahari ya Mediterania.
[e]**9:2** 2Nya 20:1; Mit 11:11; Isa 8:9-12; Yoe 3:9-12; Mdo 4:26-28
[f]**9:2** 1Nya 8:29; 14:16; 16:19; 21:29; 2Nya 1:2; Neh 3:7; Isa 28:21; Yer 28:1; 41:12; Mwa 12:8; Yos 8:1
[g]**9:3** Yos 10:10; 11:19; 18:25; 21:17; 2Sam 2:21; 5:25; 20:8; 1Fal 3:4
[h]**9:6** Kum 11:30; Mwa 26:28; Yos 5:10
[i]**9:7** Kut 23:32; 1Fal 5:12; Yos 11:19; Kum 7:2
[j]**9:8** Kum 20:11; 2Fal 10:5
[k]**9:9** Kum 20:15; Hes 23:22; Yos 2:9; Ay 32:19; Mt 9:17; Lk 5:37-38; Amu 2:2
[l]**9:10** Hes 21:24-25; 21:33-35; Yos 2:10
[m]**9:14** Kut 16:28; Hes 27:21; 1Sam 22:10; 2Sam 5:19; Isa 30:1-2
[n]**9:15** Yos 10:1, 4; 11:19; 2Sam 21:2; 24:1; Amu 1:21; Za 106:34; Kut 23:32
[o]**9:17** Yos 18:25; 2Sam 4:2; 23:37; Yos 15:9; 18:14-15; Amu 18:12; 1Sam 6:21; 7:2; Za 132:6; Yer 26:20

wana wa Israeli wakasafiri na siku ya tatu
wakafika kwenye miji yao ya Gibeoni,
Kefira, Beerothi na Kiriath-Yearimu.
18 [a]Lakini Waisraeli hawakuwashambulia
kwa kuwa viongozi wa kusanyiko walikuwa
wamewaapia kwa BWANA, Mungu wa
Israeli.

Kusanyiko lote likanung'unika dhidi
ya hao viongozi, 19 lakini viongozi wote
wakawajibu, "Tumeshawaapia kwa
BWANA, Mungu wa Israeli, kwa hiyo
hatuwezi kuwagusa sasa. 20 [b]Hivi ndivyo
tutakavyowafanyia: Tutawaacha waishi, ili
ghadhabu isije juu yetu kwa kuvunja kiapo
tulichowaapia." 21 [c]Wakaendelea kusema,
"Waacheni waishi, lakini wawe wapasua
kuni na wachota maji kwa ajili ya jamii
yote." Hivyo ahadi waliyoweka viongozi
kwao ikawa hivyo.

22 Kisha Yoshua akawaita Wagibeoni na
kuwaambia, "Kwa nini mmetudanganya
kwa kutuambia, 'Tunaishi mbali nanyi,'
wakati ambapo ninyi mnaishi karibu nasi?
23 [d]Sasa mko chini ya laana: Daima mtakuwa
wapasua kuni na wachota maji kwa ajili ya
nyumba ya Mungu wangu."

24 Wakamjibu Yoshua, "Watumwa
wako waliambiwa waziwazi jinsi BWANA
Mungu wenu alivyomwamuru mtumishi
wake Mose kuwapa ninyi nchi hii yote na
kuwaangamiza wakazi wake wote toka
mbele zenu. Kwa hiyo tuliogopa mno
kwa ajili ya uhai wetu kwa sababu yenu,
ndiyo maana tukafanya neno hili. 25 [e]Sasa
tupo mikononi mwako. Tufanyieni lolote
mnaloona kuwa jema na haki kwako."

26 Kwa hiyo Yoshua akawaokoa mikononi
mwa Waisraeli, nao hawakuuawa. 27 [f]Siku
hiyo Yoshua akawafanya Wagibeoni
wapasua kuni na wachota maji kwa ajili ya
jamii na kwa ajili ya madhabahu ya BWANA
mahali pale ambapo BWANA angepachagua.
Hivyo ndivyo walivyo hadi hivi leo.

*Jua Linasimama*

10 [g]Baada ya haya Adoni-Sedeki mfalme
wa Yerusalemu alisikia kuwa Yoshua
alikuwa ameteka mji wa Ai na kuuangamiza
kabisa, tena alikuwa ameua mfalme wake,
kama alivyofanya huko Yeriko na mfalme
wake, tena ya kuwa watu wa Gibeoni
walikuwa wamefanya mapatano ya amani
na Waisraeli, na walikuwa wakiishi karibu
yao. 2 [h]Yeye na watu wake wakataharuki
mno kwa kuwa Gibeoni ulikuwa mji
mkubwa kama mmojawapo ya miji ya
kifalme; ulikuwa mkubwa kuliko Ai, nao
watu wake wote walikuwa mashujaa wa
vita. 3 [i]Hivyo Adoni-Sedeki mfalme wa
Yerusalemu akaomba msaada kwa Hohamu
mfalme wa Hebroni, Piramu mfalme wa
Yarmuthi, Yafia mfalme wa Lakishi, na
Debiri mfalme wa Egloni. 4 [j]Akawaambia,
"Njooni mnisaidie kuipiga Gibeoni, kwa
sababu imefanya mapatano ya amani na
Yoshua na Waisraeli."

5 [k]Ndipo hao wafalme watano wa
Waamori, ambao ni wafalme wa Yerusalemu,
Hebroni, Yarmuthi, Lakishi na Egloni,
wakaunganisha majeshi yao. Wakapanda na
vikosi vyao vyote, nao wakajipanga dhidi
ya Gibeoni na kuishambulia.

6 [l]Nao Wagibeoni wakatuma ujumbe
kwa Yoshua kwenye kambi ya Gilgali na
kumwambia, "Usiwatelekeze watumishi
wako. Panda haraka uje kwetu kutuokoa!
Tusaidie, kwa sababu wafalme wote wa
Waamori wakaao kwenye nchi ya vilima

---

[a]**9:18** Amu 21:1, 7, 18; 1Sam 20:17; Za 15:4; Kut 15:24
[b]**9:20** Mwa 24:8; Eze 17:13-18; Zek 5:3-4
[c]**9:21** Kum 29:11
[d]**9:23** Mwa 9:25
[e]**9:25** Mwa 16:6; Yer 26:14; Kut 23:32; Kum 20:15-17; Kut 15:14
[f]**9:27** Kut 1:11; Kum 29:11; 12:5; 1Fal 8:29; 2Nya 7:12, 20; Za 78:68

[g]**10:1** Yos 12:10; 15:8, 63; 18:28; Amu 1:7; Yos 8:1; Kum 20:16; Yos 8:22; 9:3, 15
[h]**10:2** Kut 15:14-16; Kum 11:25; 28:10; Za 48:4-6; Mit 1:26, 27; Ebr 10:27, 31; Ufu 6:15-17
[i]**10:3** Mwa 13:18; Yos 12:11; 15:35; 21:29; Neh 11:29; Yos 12:11; 15:39; 2Fal 14:19; 2Nya 11:9; 25:27; 32:9; Neh 11:30; Isa 32:6; 37:8; Yer 34:7; Mik 1:13
[j]**10:4** Yos 9:15
[k]**10:5** Hes 13:29; Kum 1:7; Yos 9:2
[l]**10:6** Kum 11:30

wameunganisha majeshi yao pamoja dhidi
yetu."
7 [a]Basi Yoshua akaondoka Gilgali
pamoja na jeshi lake lote, wakiwepo
watu wote mashujaa wa vita. 8 [b]BWANA
akamwambia Yoshua, "Usiwaogope watu
hao, nimewatia mkononi mwako. Hakuna
yeyote atakayeweza kushindana nawe."
9 Baada ya Yoshua kutembea usiku
kucha kutoka Gilgali, akawashambulia
ghafula. 10 [c]BWANA akawafadhaisha
mbele ya Waisraeli, nao wakawashinda
kwa ushindi mkuu huko Gibeoni. Israeli
wakawafukuza kuelekea njia iendayo
Beth-Horoni wakiwaua mpaka kufikia njia
iendayo Azeka na Makeda. 11 [d]Walipokuwa
wakikimbia mbele ya Israeli kwenye
barabara iteremkayo kutoka Beth-Horoni
hadi Azeka, BWANA akawavumishia mawe
makubwa ya mvua kutoka mbinguni, na
wengi wao wakauawa na hayo mawe kuliko
wale waliouawa kwa upanga wa Waisraeli.
12 [e]Katika siku ile ambayo BWANA
aliwapeana Waamori kwa Israeli, Yoshua
akanena na BWANA akiwa mbele ya
Waisraeli akasema:

"Wewe jua, simama juu ya Gibeoni,
  wewe mwezi, tulia juu ya Bonde la
    Aiyaloni."
13 [f]Hivyo jua likasimama,
  nao mwezi ukatulia,
hadi taifa hilo lilipokwisha
  kujilipizia kisasi kwa adui wake,

kama ilivyoandikwa katika Kitabu cha
Yashari.
Jua likasimama kimya katikati ya
mbingu, likachelewa kuzama muda wa siku
moja nzima. 14 [g]Haijakuwepo siku nyingine
kama hiyo kabla au baada, siku ambayo
BWANA alimsikiliza mwanadamu. Hakika
BWANA alikuwa akiwapigania Israeli.
15 Ndipo Yoshua akarudi kambini huko
Gilgali pamoja na Israeli yote.

### *Wafalme Watano Wa Waamori Wauawa*

16 [h]Basi wale wafalme watano wakawa
wamekimbia kujificha kwenye pango huko
Makeda. 17 Yoshua alipoambiwa kuwa
wafalme hao watano wamekutwa wakiwa
wamejificha ndani ya pango huko Makeda,
18 akasema, "Vingirisheni mawe makubwa
kwenye mdomo wa hilo pango, tena wekeni
walinzi wa kulilinda. 19 Lakini msiwaache!
Wafuatieni adui zenu, washambulieni
kutoka nyuma, wala msiwaache wafike
kwenye miji yao, kwa kuwa BWANA Mungu
wenu amewatia mkononi mwenu."
20 [i]Hivyo Yoshua pamoja na Waisraeli
wakawaangamiza kabisa karibu wote,
lakini wachache waliosalia walifika kwenye
miji yao yenye maboma. 21 Basi jeshi lote
likarudi salama kwa Yoshua huko kambini
Makeda, na hakuna yeyote aliyetoa neno
kinyume cha Waisraeli.
22 Ndipo Yoshua akasema, "Haya
fungueni mdomo wa pango, mniletee hao
wafalme watano." 23 Kwa hiyo wakawatoa
hao wafalme watano nje ya pango: wafalme
wa Yerusalemu, Hebroni, Yarmuthi, Lakishi
na Egloni. 24 [j]Walipokuwa wamewaleta
hawa wafalme kwa Yoshua, akawaita watu
wote wa Israeli, na kuwaambia majemadari
wa vita waliokwenda pamoja naye, "Njooni
hapa mweke nyayo zenu juu ya shingo za
hawa wafalme." Basi wakaja wakaweka
nyayo zao shingoni.

[a]**10:7** Yos 8:1
[b]**10:8** Kum 3:2; Yos 1:9; 2:24; Kum 7:24; 7:24; 11:25; Yos 11:6; 23:9; Amu 4:14
[c]**10:10** Kut 14:24; Kum 7:23; Yos 9:3; 16:3-5; 18:13-14; 21:22; 1Fal 9:17; 1Nya 6:68; 7:24; 2Nya 8:5; 25:13; Yos 15:35; 1Sam 17:1; 2Nya 11:9; Neh 11:30; Yer 34:7; Yos 12:16; 15:41
[d]**10:11** Kut 9:18; Za 18:12; Isa 28:2; 17; 32:19; Eze 13:11; Amu 5:20
[e]**10:12** Amo 2:9; Yos 19:42; 21:24; Amu 1:35; 12:12; 1Sam 14:31; 1Nya 6:69; 8:13; 2Nya 11:10; 28:18
[f]**10:13** Hab 3:11; 2Sam 1:18; Isa 38:8
[g]**10:14** Yos 10:42; Kut 14:14; Za 106:43; 136:24; Isa 63:10; Yer 21:5; Isa 38:8; Kum 1:30; 3:22; 20:4; 33:29; Amu 1:19, 22; 2Nya 20:29; Neh 4:20; Isa 31:4; Zek 12:3
[h]**10:16** Za 68:12
[i]**10:20** Kum 20:16; 2Nya 11:10; Yer 4:5; 5:17; 8:14; 35:11
[j]**10:24** Kum 7:24; Mal 4:3; 2Sam 22:40; Za 110:1; Isa 51:23

25 [a]Yoshua akawaambia, “Msiogope, wala
msivunjike moyo. Kuweni hodari na wenye
ushujaa. Hili ndilo BWANA atakalowatendea
adui zenu wote mnaokwenda kupigana nao.”
26 [b]Ndipo Yoshua akawapiga na kuwaua
wale wafalme na kuwatundika juu ya miti
mitano, nao wakaachwa wakining’inia juu
ya ile miti hadi jioni.
27 [c]Wakati wa kuzama jua Yoshua
akaamuru, nao wakawashusha kutoka
kwenye ile miti na kuwatupa kwenye lile
pango ambalo walikuwa wamejificha.
Kwenye mdomo wa lile pango wakaweka
mawe makubwa, ambayo yapo hadi leo.
28 [d]Siku ile Yoshua akateka Makeda.
Akamuua kila mmoja katika ule mji, pamoja
na mfalme wake kwa upanga. Hakubakiza
mtu yeyote. Akamfanyia mfalme wa
Makeda kama vile alivyokuwa amemfanyia
mfalme wa Yeriko.

*Israeli Yaangamiza Miji Ya Kusini*

29 [e]Ndipo Yoshua akaondoka Makeda
akiwa pamoja na Israeli yote mpaka mji
wa Libna na kuushambulia.
30 BWANA
pia akautia huo mji wa Libna pamoja na
mfalme wake mikononi mwa Israeli. Yoshua
akaangamiza ule mji na kila mtu aliyekuwa
ndani yake kwa upanga. Hakubakiza huko
mtu yeyote. Akamfanyia mfalme wa Libna
kama alivyokuwa amemfanyia mfalme wa
Yeriko.
31 [f]Kisha Yoshua akaondoka Libna
kwenda Lakishi akiwa pamoja na
Israeli yote; wakajipanga dhidi yake na
kuushambulia.
32 BWANA akautia Lakishi
mikononi mwa Israeli, Yoshua akauteka
siku ya pili. Yoshua akauangamiza mji na
kila kilichokuwa ndani yake kwa upanga,
kama tu vile alivyokuwa ameufanyia mji wa
Libna.
33 [g]Wakati huo huo, Horamu mfalme
wa Gezeri alikuwa amepanda ili kusaidia
Lakishi, lakini Yoshua akamshinda pamoja
na jeshi lake, hadi hapakubakia mtu yeyote.
34 Ndipo Yoshua akaondoka Lakishi
kwenda Egloni akiwa pamoja na Israeli yote;
wakajipanga dhidi yake na kuushambulia.
35 [h]Wakauteka mji huo siku ile ile,
wakaupiga kwa upanga na kumwangamiza
kila mmoja aliyekuwa ndani yake, kama
vile walivyokuwa wameufanyia Lakishi.
36 [i]Kisha Yoshua akapanda kutoka Egloni
kwenda Hebroni akiwa pamoja na Israeli
yote na kuushambulia.
37 Wakauteka mji na
kuupiga kwa upanga, pamoja na mfalme
wake, vijiji vyake na kila mmoja aliyekuwa
ndani yake. Hawakubakiza mtu yeyote.
Kama vile huko Egloni, waliuangamiza
kabisa pamoja na kila mmoja aliyekuwa
ndani yake.
38 [j]Ndipo Yoshua na Israeli wote
wakageuka na kuushambulia Debiri.
39 Wakauteka mji, mfalme wake na vijiji
vyake, na kuupiga kwa upanga. Kila mmoja
aliyekuwa ndani yake wakamwangamiza
kabisa. Hawakubakiza mtu yeyote.
Wakaufanyia Debiri na mfalme wake kama
vile walivyokuwa wameifanyia miji ya
Libna na Hebroni na wafalme wao.
40 [k]Hivyo Yoshua akalishinda eneo hilo
lote, ikiwa ni pamoja na nchi ya vilima,
na Negebu, na sehemu ya magharibi chini
ya vilima, materemko ya milima, pamoja
na wafalme wake wote. Hakubakiza mtu
yeyote. Akaangamiza kabisa kila kitu
chenye pumzi, kama vile BWANA, Mungu wa
Israeli, alivyokuwa ameamuru.
41 [l]Yoshua
akawashinda kuanzia Kadesh-Barnea hadi
Gaza na kutoka eneo lote la Gosheni hadi

[a]**10:25** Kum 31:6; 1Sam 17:37; Za 63:9; 2Tim 4:17; Kum 3:21; 7:19
[b]**10:26** Hes 25:14; Yos 8:29; 2Sam 21:6-9; Es 2:23; Za 149:7-9
[c]**10:27** Kum 21:23; Mwa 35:20; Yos 8:9, 29
[d]**10:28** Kum 20:16; Yos 6:21
[e]**10:29** Hes 33:20; Yos 15:42; 21:13; 2Fal 8:22; 19:8
[f]**10:31** 2Fal 14:19; Mik 1:13
[g]**10:33** Yos 12:12; 16:3, 10; 21:21; Amu 1:29; 2Sam 5:25; 1Fal 9:15; 1Nya 6:67
[h]**10:35** Hes 13:22; Amu 1:10; 2Sam 5:14
[i]**10:36** Mwa 13:18; Yos 14:13; 15:13; 20:7; 21:11; Amu 16:3
[j]**10:38** Yos 15:15; Amu 1:11
[k]**10:40** Mwa 12:9; Yos 12:8; 15:19-21; 18:25; 1Sam 30:27; Kum 1:7; 7:24; 20:16-17; Yos 15:21-63; 19:1-8; Kut 23:31-33
[l]**10:41** Mwa 14:17; 10:19; Yos 11:16; 15:51; Hes 13:17; 32:8; Kum 2:23

Gibeoni. 42 [a]Wafalme hawa wote pamoja na
nchi zao Yoshua aliwashinda kwa wakati
mmoja, kwa sababu BWANA, Mungu wa
Israeli, aliwapigania Israeli.
43 [b]Ndipo Yoshua akarudi pamoja na
Israeli yote kwenye kambi huko Gilgali.

*Wafalme Wa Kaskazini Washindwa*

11 [c]Ikawa Yabini mfalme wa Hazori
aliposikia habari za mambo haya,
akatuma ujumbe kwa Yobabu mfalme wa
Madoni, na kwa mfalme wa Shimroni, na
kwa mfalme wa Akishafu, 2 [d]na pia kwa
wafalme wa upande wa kaskazini wale
waliokuwa milimani, katika Araba upande
wa kusini mwa Kinerethi, kwenye shefela,
upande wa magharibi na katika miinuko
ya Nafoth-Dori upande wa magharibi;
3 [e]kwa Wakanaani upande wa mashariki na
magharibi; kwa Waamori, Wahiti, Waperizi
na Wayebusi katika nchi ya vilima; na kwa
Wahivi chini ya Hermoni katika eneo ya
Mispa. 4 [f]Wakaja na vikosi vyao vyote
na hesabu kubwa ya farasi na magari ya
kuvutwa na farasi, jeshi kubwa, kama
wingi wa mchanga ulio pwani ya bahari.
5 [g]Wafalme hawa wote wakaunganisha
majeshi yao na kupiga kambi pamoja
kwenye Maji ya Meromu, ili kupigana dhidi
ya Israeli.
6 [h]BWANA akamwambia Yoshua,
"Usiwaogope, kwa sababu kesho saa kama
hii nitawatia wote mikononi mwa Israeli,
wakiwa wameuawa. Utakata mishipa
ya nyuma ya miguu ya farasi wao na
kuyachoma moto magari yao ya vita."
7 Hivyo Yoshua pamoja na jeshi lake
lote wakaja dhidi yao ghafula kwenye
Maji ya Meromu kuwashambulia, 8 [i]naye
BWANA akawatia mikononi mwa Israeli.
Wakawashinda na kuwafukuza hadi Sidoni
Kuu na kuwafikisha Misrefoth-Maimu, hadi
Bonde la Mispa upande wa mashariki, hadi
pakawa hakuna yeyote aliyebaki. 9 Yoshua
akawatendea kama BWANA alivyoamuru.
Akakata mishipa ya nyuma ya miguu ya
farasi wao na kuchoma moto magari yao
ya vita.
10 [j]Wakati huo Yoshua akarudi na kuuteka
mji wa Hazori na kumuua mfalme wake
kwa upanga. (Hazori ulikuwa mji mkuu
wa falme hizo zote.) 11 [k]Kila aliyekuwa
ndani yake wakamuua kwa upanga.
Wakawaangamiza kabisa, wala hawakusaza
chochote chenye pumzi na akauchoma
Hazori kwenyewe kwa moto.
12 [l]Yoshua akaiteka hii miji yote ya kifalme
pamoja na wafalme wake na kuwapiga kwa
upanga. Akawaangamiza kabisa wote, jinsi
Mose mtumishi wa BWANA alivyowaagiza.
13 Lakini Israeli hawakuichoma moto hata
mojawapo ya miji iliyojengwa katika
vilima vyao vidogo isipokuwa mji wa
Hazori ambao Yoshua aliuchoma moto.
14 [m]Waisraeli wakajichukulia nyara zote na
mifugo yote ya miji hii, bali waliwaua watu
wote kwa upanga hadi walipowaangamiza
kabisa, pasipo kumbakiza yeyote mwenye
pumzi. 15 [n]Kama vile BWANA alivyomwagiza
Mose mtumishi wake, vivyo hivyo Mose
alimwagiza Yoshua, naye Yoshua akafanya
kama vivyo, hakukosa kufanya lolote katika
yale yote BWANA aliyomwagiza Mose.
16 [o]Yoshua akaiteka nchi hii yote: nchi ya
vilima, Negebu yote, eneo yote ya Gosheni,
shefela ya upande wa magharibi, Araba
na milima ya Israeli pamoja na shefela

---

[a]**10:42** Yos 10:14; Za 44:2; 80:8
[b]**10:43** Yos 5:9; 1Sam 11:14; 13:12
[c]**11:1** Amu 4:2, 7, 23; Za 83:9; Yos 12:19; 15:23-25; 19:36; 1Sam 12:9; 1Fal 9:15; 2Fal 15:29; Neh 11:33; Yer 49:28, 33; Yos 12:20; 19:25
[d]**11:2** Yos 12:1; 18:18; Hes 34:11; Kum 3:17; Yos 19:35; 1Fal 15:20; Yos 12:23; 17:11; Amu 1:27; 1Fal 4:11; 1Nya 7:29
[e]**11:3** Yos 3:10; Hes 13:17; Kut 3:8; Kum 7:1; Amu 3:3-5; 1Fal 9:20; Kum 3:8; Mwa 31:49; Yos 15:38; 18:26; Amu 11:11; 20:1; 21:1; 1Sam 7:5-6; 1Fal 15:22; 2Fal 25:23
[f]**11:4** Mwa 12:2; Amu 7:12; 1Sam 13:5; Mwa 22:17; 32:12
[g]**11:5** Amu 5:19
[h]**11:6** Yos 2:24; Mwa 49:6
[i]**11:8** Mwa 10:15; Amu 18:7; Yos 13:6
[j]**11:10** Isa 3:25; Yer 41:2; 44:18
[k]**11:11** Kum 7:2; 20:16-17; Hes 31:10
[l]**11:12** Hes 33:50-52; Kum 7:2
[m]**11:14** Kum 20:16; Mwa 22:17; 32:12
[n]**11:15** Kut 34:11; Kum 7:2; Yos 1:7
[o]**11:16** Hes 13:17; Kum 1:7; Yos 10:41

zao, 17 [a]kuanzia Mlima Halaki ambao
umeinuka kuelekea Seiri hadi Baal-Gadi
katika Bonde la Lebanoni chini ya Mlima
Hermoni. Akawateka wafalme wake wote,
akawapiga na kuwaua. 18 Yoshua akapigana
vita dhidi ya wafalme hawa wote kwa
muda mrefu. 19 [b]Hakuna mji wowote katika
eneo hili uliofanya mkataba wa amani na
Israeli, isipokuwa hao Wahivi wa Gibeoni.
Wengine wote walishindwa katika vita.
20 [c]Kwa maana BWANA mwenyewe ndiye
aliifanya mioyo yao iwe migumu, ili
kupigana vita dhidi ya Israeli ili apate
kuwafutilia mbali pasipo huruma, kama
BWANA alivyomwagiza Mose.
21 [d]Wakati huo Yoshua akaenda
kuwaangamiza Waanaki kutoka nchi ya
vilima: kuanzia Hebroni, Debiri na Anabu,
na kutoka nchi yote ya vilima ya Yuda
na kutoka nchi yote ya vilima ya Israeli.
Yoshua akawaangamiza kabisa pamoja na
miji yao. 22 [e]Hawakubaki Waanaki wowote
katika nchi ya Israeli, ila tu katika nchi ya
Gaza, Gathi na Ashdodi. 23 [f]Hivyo Yoshua
akaiteka nchi hiyo yote kama vile BWANA
alivyokuwa amemwagiza Mose, naye
Yoshua akawapa Israeli kuwa urithi wao,
kulingana na walivyogawanyika katika
kabila zao.

Ndipo nchi ikawa na amani bila vita.

*Orodha Ya Wafalme Walioshindwa*

12 [g]Hawa ndio wafalme wa nchi ambao
Waisraeli waliwashinda na kuitwaa
nchi yao upande wa mashariki mwa
Yordani, kuanzia Bonde la Arnoni mpaka
Mlima Hermoni, pamoja na eneo lote la
upande wa mashariki ya Araba:

2 [h]Sihoni mfalme wa Waamori, ambaye
alitawala huko Heshboni.

Alitawala kuanzia Aroeri kwenye
ukingo wa Bonde la Arnoni, kuanzia
katikati ya bonde, hadi kwenye Mto
Yaboki, ambao ni mpaka wa Waamoni.
Hii ilijumlisha nusu ya Gileadi. 3 [i]Pia
alitawala Araba ya mashariki kuanzia
Bahari ya Kinerethi[j] hadi Bahari ya
Araba (yaani Bahari ya Chumvi[k]), hadi
Beth-Yeshimothi, kisha kuelekea kusini
chini ya materemko ya Pisga.

4 [l]Nayo nchi ya Ogu mfalme wa Bashani,
aliyekuwa mmoja wa mabaki ya Warefai,
aliyetawala Ashtarothi na Edrei.

5 [m]Naye alitawala katika Mlima
Hermoni, Saleka, Bashani yote hadi
mpaka wa watu wa Geshuri, na watu
wa Maaka na nusu ya Gileadi, hadi
kwenye mpaka wa Sihoni mfalme wa
Heshboni.

6 [n]Mose, mtumishi wa BWANA, na
Waisraeli wakawashinda. Naye Mose
mtumishi wa BWANA akawapa Wareubeni,
Wagadi na nusu ya kabila la Manase nchi
ya hao wafalme ili iwe milki yao.

7 [o]Hawa ndio wafalme wa nchi ambao
Yoshua na Waisraeli waliwashinda upande
wa magharibi mwa Yordani, kuanzia Baal-
Gadi katika Bonde la Lebanoni hadi kufikia
Mlima Halaki, unaoinuka ukielekea Seiri.

---

[a]**11:17** Mwa 14:6; Hes 24:18; Kum 33:2; Yos 13:5; Kum 3:25; Yos 12:7-8; Kum 3:9; 7:24
[b]**11:19** Yos 9:1-3; 9:15
[c]**11:20** Kut 4:21; Rum 9:18; Kut 14:17; Kum 7:16; Amu 14:4; Kum 2:30; 1Sam 2:25; 1Fal 12:15; 22:20-23; Yak 1:13-17; Kum 20:16
[d]**11:21** Hes 13:22, 33; Yos 10:3; 15:50; Kum 9:2; Amu 1:10; Yer 3:23
[e]**11:22** Mwa 10:19; Yos 12:17; 19:13; 1Sam 5:8; 17:4; 1Fal 2:39; 2Fal 14:25; 1Nya 8:13; Amo 6:2; Yos 15:47; 1Sam 5:1; Isa 20:1
[f]**11:23** Yos 21:43-45; Neh 9:24; Kum 1:38; 12:9-10; 25:19; Yos 13:7; Hes 26:53; Za 105:44; Kut 33:14; Yos 14:15
[g]**12:1** Za 136:21; Hes 32:19; 21:13; Kum 3:8; Yos 11:2
[h]**12:2** Yos 12:5; Hes 21:21-25; Yos 13:10; Amu 11:19; Hes 32:34; Yos 13:16; Mwa 19:38; 31:21; 32:22; Hes 32:26; Kum 2:36; 3:15; Yos 13:11, 25; 17:1; 20:8; 21:38; Amu 5:17; 7:3; 10:8
[i]**12:3** Yos 11:2; Mwa 14:3; Hes 33:49; Yos 13:20; Hes 21:20
[j]3 Yaani Bahari ya Galilaya.
[k]3 Yaani Bahari Mfu.
[l]**12:4** Hes 21:21; 33; Yos 13:30; Mwa 14:5; Kum 1:4
[m]**12:5** Kum 3:10; Hes 32:33; Yos 17:1; 20:8; 21:27; 22:7; 13:2, 13; 1Sam 27:8; Kum 3:14
[n]**12:6** Kum 3:8; Hes 32:29-33; Yos 13:8
[o]**12:7** Yos 11:17

(Yoshua alitoa nchi zao kwa makabila
ya Israeli iwe urithi wao sawasawa na
mgawanyiko wa makabila yao: 8 [a]nchi ya
vilima, shefela, upande wa magharibi,
Araba, materemko ya milima, jangwa,
na Negebu; nchi za Wahiti, Waamori,
Wakanaani, Waperizi, Wahivi na Wayebusi):

9 [b]mfalme wa Yeriko mmoja
mfalme wa Ai (karibu na Betheli) mmoja
10 [c]mfalme wa Yerusalemu mmoja
mfalme wa Hebroni mmoja
11 [d]mfalme wa Yarmuthi mmoja
mfalme wa Lakishi mmoja
12 [e]mfalme wa Egloni mmoja
mfalme wa Gezeri mmoja
13 mfalme wa Debiri mmoja
mfalme wa Gederi mmoja
14 [f]mfalme wa Horma mmoja
mfalme wa Aradi mmoja
15 [g]mfalme wa Libna mmoja
mfalme wa Adulamu mmoja
16 [h]mfalme wa Makeda mmoja
mfalme wa Betheli mmoja
17 [i]mfalme wa Tapua mmoja
mfalme wa Heferi mmoja
18 [j]mfalme wa Afeki mmoja
mfalme wa Lasharoni mmoja
19 [k]mfalme wa Madoni mmoja
mfalme wa Hazori mmoja
20 [l]mfalme wa Shimron-Meroni mmoja
mfalme wa Akishafu mmoja
21 [m]mfalme wa Taanaki mmoja
mfalme wa Megido mmoja
22 [n]mfalme wa Kedeshi mmoja
mfalme wa Yokneamu katika Karmeli mmoja
23 [o]mfalme wa Dori (katika Nafoth-Dori) [p] mmoja
mfalme wa Goimu katika Gilgali mmoja
24 [q]mfalme wa Tirsa mmoja

wafalme jumla yao ilikuwa thelathini na
mmoja.

*Sehemu Za Kanaani Ambazo Hazijatwaliwa*

13 [r]Yoshua alipokuwa mzee na umri
wake ukiwa umesogea sana, Bwana
akamwambia, “Wewe ni mzee sana, na
bado kumesalia sehemu kubwa sana za
nchi ambazo ni za kutwaliwa.

2 [s]“Nchi iliyosalia ni hii: maeneo yote ya
Wafilisti na Wageshuri: 3 [t]kutoka Mto
Shihori ulioko mashariki mwa Misri,
kuelekea kaskazini kwenye eneo la
Ekroni, ambayo yote ilihesabika kama
ya Wakanaani (maeneo yale matano ya
watawala wa Kifilisti, ambayo ni Gaza,
Ashdodi, Ashkeloni, Gathi na Ekroni:
ndiyo nchi ya Waavi); 4 kuanzia kusini,
nchi yote ya Wakanaani, kuanzia Ara
ambayo ni ya Wasidoni, ikienea hadi
Afeki, na eneo la Waamori, 5 [u]eneo la
Wagebali;[v] Lebanoni yote kuelekea

[a]**12:8** Ezr 9:1; Kum 1:7; Yos 3:10; 11:17
[b]**12:9** Hes 33:48; Mwa 12:8; Yos 8:1; 7:2; 8:9; 18:13; Amu 1:23; 4:4; 20:18; 21:2; Neh 11:31
[c]**12:10** Yos 10:1
[d]**12:11** Yos 10:3
[e]**12:12** Yos 10:3, 33
[f]**12:14** Hes 14:45; 21:1
[g]**12:15** Hes 33:20; Mwa 38:1; Yos 15:35; Mik 1:15
[h]**12:16** Yos 10:10; 7:2
[i]**12:17** Yos 15:34; 16:8; 17:8; 11:22; 1Fal 4:10
[j]**12:18** Yos 13:4; 19:30; Amu 1:31; 1Sam 4:1; 29:1
[k]**12:19** Yos 11:1
[l]**12:20** Yos 11:1
[m]**12:21** Yos 17:11; 21:25; Amu 1:27; 5:19; 1Fal 4:12
[n]**12:22** Yos 15:23; 19:37; 20:7; 21:32; Amu 4:6-9; Yos 19:11; 21:34; 15:55; 19:26; 1Sam 15:12; 2Sam 23:35
[o]**12:23** Yos 11:2
[p]23 Au: katika miinuko ya Nafoth-Dori.
[q]**12:24** 1Fal 14:17; 15:33; 16:8, 23; Wim 6:4; Za 135:11; 136:18
[r]**13:1** Mwa 24:1; Yos 14:10; 23:1-3; 1Fal 1:1
[s]**13:2** Mwa 10:14; Amu 3:31; Yos 12:5
[t]**13:3** 1Nya 13:5; Isa 23:3; Yer 2:18; Yos 15:11; 19:43; Amu 1:18; 1Sam 5:10; 7:14; Amu 3:3; 16:5, 18; 1Sam 6:4, 17; Isa 14:29; Eze 25:15; Yos 11:22; Amo 3:9; Amu 14:19; 2Sam 1:20; Kum 2:23; 13:4; Yos 12:18; Mwa 14:7; 15:16
[u]**13:5** 1Fal 5:18; Za 83:7; Eze 27:9; Yos 11:17; Kum 3:8; Hes 13:21; 34:8; Amu 3:3
[v]5 Yaani eneo la Bubilo, mji wa zamani sana wa Ufoinike (kama kilomita 80 kaskazini mwa Beiruti).

mashariki, kuanzia Baal-Gadi chini ya
Mlima Hermoni hadi Lebo-Hamathi.

6 [a]"Na kuhusu wakaaji wote katika maeneo ya milima, kuanzia Lebanoni hadi Misrefoth-Maimu, pamoja na eneo lote la Wasidoni, mimi mwenyewe nitawafukuza watoke mbele ya Waisraeli. Hakikisha umegawa nchi hii kwa Israeli kuwa urithi,
kama nilivyokuagiza, 7 [b]sasa basi, ligawanye
eneo hili kwa yale makabila tisa na ile nusu ya kabila la Manase kuwa urithi."

*Mgawanyo Wa Nchi Mashariki Mwa Yordani*

8 [c]Ile nusu nyingine ya Manase, Wareubeni na Wagadi, walishapokea urithi Mose aliokuwa amewapa mashariki mwa Yordani, sawasawa na mtumishi wa BWANA alivyowagawia.

9 [d]Eneo lao lilienea toka Aroeri,
iliyoko ukingoni mwa Bonde la
Arnoni kuanzia mji ulio katikati ya
bonde, likijumlisha nchi ya uwanda
wa juu wote wa Medeba mpaka Diboni,
10 [e]nayo miji yote ya Sihoni mfalme wa
Waamori, aliyetawala Heshboni, hadi
mpakani mwa Waamoni. 11 [f]Vilevile
ilijumlisha Gileadi, eneo la Wageshuri
na Wamaaka, mlima wote wa Hermoni
na Bashani yote ikienea hadi Saleka:
12 [g]yaani ufalme wote wa Ogu katika
Bashani, aliyekuwa ametawala katika
Ashtarothi na Edrei, na ndiye pekee
alisalia kwa Warefai. Mose alikuwa
amewashinda na kuteka nchi yao.
13 [h]Lakini Waisraeli hawakuwafukuza
watu wa Geshuri na wa Maaka, kwa
hiyo wanaendelea kuishi miongoni
mwa Waisraeli mpaka leo hii.

14 [i]Lakini kwa kabila la Lawi, Mose hakupeana urithi, kwa kuwa sadaka za kuteketezwa kwa moto zilizotolewa kwa BWANA, Mungu wa Israeli, ndizo zilizokuwa urithi wao, kama alivyowaahidi.

15 Haya ndiyo maeneo ambayo Mose alikuwa amewapa kabila la Reubeni ukoo kwa ukoo:

16 [j]Eneo la Aroeri lililo ukingoni mwa
Bonde la Arnoni, na kuanzia mji ulio
katikati ya bonde, pia uwanda wote wa
juu kupita Medeba 17 [k]hadi Heshboni
na miji yake yote kwenye uwanda
wa juu, ikijumlishwa miji ya Diboni,
Bamoth-Baali, Beth-Baal-Meoni,
18 [l]Yahasa, Kedemothi, Mefaathi,
19 [m]Kiriathaimu, Sibma, Sereth-Shahari
juu ya kilima kilicho katika bonde,
20 [n]Beth-Peori, materemko ya Pisga
na Beth-Yeshimothi: 21 [o]miji yote ya
uwanda wa juu na eneo lote la utawala
wa Sihoni mfalme wa Waamori,
aliyetawala katika Heshboni. Mose
alikuwa amemshinda Sihoni, pia
watawala wakuu wa Wamidiani,
ambao ni Evi, Rekemu, Suri, Huri na
Reba, waliokuwa wameungana na
Sihoni, ambao waliishi katika nchi ile.
22 [p]Pamoja na wale waliouawa katika
vita, Waisraeli walikuwa wamemuua
kwa upanga Balaamu mwana wa
Beori aliyekuwa mchawi. 23 [q]Mpaka
wa Wareubeni ulikuwa ni ukingo wa
Mto Yordani. Miji hii na vijiji vyake

[a]**13:6** Yos 11:8; Za 80:8; Hes 33:54; 34:13; Amu 2:12; Yos 14:1, 2
[b]**13:7** Yos 11:23; Za 78:55
[c]**13:8** Yos 12:6; 18:7; Hes 32:33; Kum 3:12; Yos 12:6; 18:7
[d]**13:9** Hes 32:34; Kum 2:36; Amu 11:26; 2Sam 24:5; Yer 48:8, 21; Hes 21:30; 32:3; Isa 15:2
[e]**13:10** Yos 12:2; Hes 21:24
[f]**13:11** Yos 12:2-5
[g]**13:12** Kum 1:4; Yos 12:4; Mwa 14:5; Kum 3:5, 11; Hes 21:24
[h]**13:13** Yos 12:5; Kum 3:12-15
[i]**13:14** Kum 18:1-2; Yos 14:2; Hes 18:20; Kum 10:9
[j]**13:16** Yos 12:2; 1Sam 30:28; Hes 21:30; Isa 15:2; Kum 3:12
[k]**13:17** Hes 32:3; 22:41; 1Nya 5:8; Yer 48:23; Eze 25:9
[l]**13:18** Hes 21:23; Kum 2:26; Yos 21:37; Yer 48:21
[m]**13:19** Hes 32:37; 32:3
[n]**13:20** Kum 3:29
[o]**13:21** Mwa 25:2; Hes 25:15; 31:8; Kum 3:10; Hes 21:24; 31:8
[p]**13:22** Hes 22:5; Mwa 30:27; Hes 23:23; 2Pet 2:15; Ufu 2:14
[q]**13:23** 1Nya 5:7

ndiyo iliyokuwa urithi wa Wareubeni
ukoo kwa ukoo.

24 Haya ndiyo maeneo ambayo Mose
alikuwa amewapa kabila la Gadi, ukoo
kwa ukoo:

25 [a]Nchi ya Yazeri, miji yote ya Gileadi
na nusu ya nchi ya Amoni iliyoenea hadi
Aroeri, karibu na Raba; 26 [b]na kuanzia
Heshboni mpaka Ramath-Mispa na
Betonimu, na kutoka Mahanaimu hadi
eneo la Debiri; 27 [c]na katika bonde,
Beth-Haramu, Beth-Nimra, Sukothi
na Safoni na sehemu iliyobaki ya
eneo la utawala wa Sihoni mfalme wa
Heshboni (upande wa mashariki mwa
Mto Yordani, eneo inayoishia kwenye
Bahari ya Kinerethi[d]). 28 [e]Miji hii na
vijiji vyake ilikuwa urithi wa kabila
la Gadi ukoo kwa ukoo.

29 Haya ndiyo maeneo ambayo Mose
alikuwa amewapa hiyo nusu ya kabila la
Manase, yaani kwa nusu ya jamaa ya uzao
wa Manase, ukoo kwa ukoo:

30 [f]Eneo lililoenea kuanzia Mahanaimu,
na kujumlisha Bashani yote, ufalme
wote wa Ogu mfalme wa Bashani,
makazi yote ya Yairi huko Bashani,
miji sitini, 31 [g]nusu ya Gileadi, na
Ashtarothi na Edrei (miji ya kifalme
ya Ogu katika Bashani). Hii ilikuwa
kwa ajili ya wazao wa Makiri mwana
wa Manase, kwa ajili ya nusu ya wana
wa Makiri, ukoo kwa ukoo.

32 [h]Huu ndio urithi alioupeana Mose
wakati alipokuwa katika tambarare za
Moabu, ng'ambo ya Yordani mashariki mwa
Yeriko. 33 [i]Lakini kwa kabila la Walawi,
Mose hakuwapa urithi; BWANA Mungu,
Mungu wa Israeli ndiye urithi wao, kama
alivyowaahidi.

*Mgawanyo Wa Nchi Magharibi Mwa Yordani*

14 [j]Basi haya ndiyo maeneo Waisraeli
waliyopokea kama urithi katika nchi ya
Kanaani, ambayo kuhani Eleazari, Yoshua
mwana wa Nuni na viongozi wa koo za
kabila za Israeli waliwagawia. 2 [k]Urithi wao
uligawanywa kwa kura kwa yale makabila
tisa na nusu, kama BWANA alivyoamuru
Mose. 3 [l]Mose alikuwa amewapa yale
makabila mawili na nusu urithi wao upande
wa mashariki mwa Yordani, lakini Walawi
hawakupewa urithi miongoni mwa hao
wengine, 4 [m]kwa kuwa wana wa Yosefu
walikuwa makabila mawili; Manase na
Efraimu. Walawi hawakupata mgawo wa
ardhi, bali walipewa miji tu kwa ajili ya
kuishi, pamoja na maeneo ya malisho kwa
ajili ya makundi yao ya kondoo, mbuzi
na ng'ombe wao. 5 [n]Kwa hiyo Waisraeli
wakagawana ile nchi, kama vile BWANA
alivyomwagiza Mose.

*Kalebu Anapewa Mji Wa Hebroni*

6 [o]Kisha watu wa Yuda wakamwendea
Yoshua huko Gilgali, naye Kalebu mwana
wa Yefune yule Mkenizi, akamwambia,
"Unajua jambo ambalo BWANA alimwambia
Mose mtu wa Mungu huko Kadesh-Barnea
kukuhusu wewe na mimi. 7 [p]Nilikuwa na
umri wa miaka arobaini, wakati Mose
mtumishi wa BWANA, aliponituma kutoka
Kadesh-Barnea kuipeleleza hiyo nchi. Nami
nikamletea taarifa kama kulingana na

[a]**13:25** Hes 21:32; Yos 21:39; 12:2; Kum 3:11; Amu 11:13; 2Sam 11:1; 12:26
[b]**13:26** Hes 21:25; Yer 49:3; Mwa 32:2; Yos 10:3
[c]**13:27** Hes 32:3; Mwa 33:17; Amu 12:1; Za 48:2; Hes 34:11; 1Fal 7:46; Kum 3:17; Yos 11:2; Mt 14:34; Lk 5:1
[d]27 Yaani Bahari ya Galilaya.
[e]**13:28** Mwa 46:16; Hes 32:3; Eze 48:27
[f]**13:30** Mwa 32:2; Hes 21:33; Yos 12:4; Hes 32:41
[g]**13:31** Hes 21:33; Mwa 50:23; Yos 17:5
[h]**13:32** Hes 26:3; 22:1
[i]**13:33** Hes 26:62; 18:20; Yos 18; 7; Eze 44:28
[j]**14:1** Yos 11:23; Za 16:6; 136:21; Kut 6:23; Yos 21:1; Hes 26:53; 34:17-18; Yos 19:51
[k]**14:2** Law 16:8; Hes 34:13; Za 16:5; Mit 16:33; 18:18
[l]**14:3** Hes 32:33; 34:14; 35:2; Yos 13:14
[m]**14:4** Mwa 41:54; Amu 1:29; Hes 35:2-3; Yos 21:2
[n]**14:5** Hes 34:13; 35:2; Yos 21:2; Eze 45:1-8; 48:8, 22
[o]**14:6** Kum 11:30; Hes 13:6; 14:30; Kum 33:1; Hes 14:38; Yos 15:17; Kum 1:19
[p]**14:7** Yos 15:6; Hes 13:17; 13:30; 14:6-9

nilivyosadiki moyoni. 8 [a]Lakini ndugu zangu
tuliopanda nao waliifanya mioyo ya watu
iyeyuke kwa hofu. Bali mimi, nilimfuata
BWANA Mungu wangu kwa moyo wote.
9 [b]Hivyo katika siku ile, Mose akaniapia,
'Nchi ambayo umeikanyaga kwa miguu
yako itakuwa urithi wako na wa watoto
wako milele, kwa sababu umemfuata
BWANA Mungu wangu kwa moyo wote.'
10 [c]"Sasa basi, kama vile BWANA
alivyoahidi, ameniweka hai kwa miaka
arobaini na mitano tangu wakati
alipomwambia Mose jambo hili, wakati
Waisraeli wakiwa wanazunguka jangwani.
Hivyo mimi hapa leo, nina umri wa miaka
themanini na mitano! 11 [d]Bado ninazo
nguvu kama siku ile Mose aliponituma.
Bado ninazo nguvu za kwenda vitani sasa
kama vile nilivyokuwa wakati ule. 12 [e]Basi
nipe nchi hii ya vilima, ambayo BWANA
aliniahidi siku ile. Wewe mwenyewe ulisikia
wakati ule kwamba Waanaki walikuwako
huko na miji yao ilikuwa mikubwa na
yenye maboma, lakini, kwa msaada wa
BWANA, nitawafukuza watoke huko kama
vile alivyonena."
13 [f]Ndipo Yoshua akambariki Kalebu
mwana wa Yefune, na akampa Hebroni
kama urithi wake. 14 [g]Hivyo Hebroni
imekuwa mali ya Kalebu mwana wa
Yefune Mkenizi tangu wakati ule, kwa
sababu alimwandama BWANA, Mungu wa
Israeli, kwa moyo wote. 15 [h](Hebroni uliitwa
Kiriath-Arba hapo mwanzo, kutokana na
huyo Arba ambaye alikuwa mtu mkuu
kupita wote miongoni mwa Waanaki.)
Kisha nchi ikawa na amani bila vita.

*Mgawo Kwa Yuda*

15 [i]Mgawo kwa kabila la Yuda, ulienea
ukoo kwa ukoo, ukishuka kufikia eneo
la Edomu, hadi Jangwa la Sini mwisho
kabisa upande wa kusini.
2 [j]Mpaka wao wa kusini ulianzia
kwenye ghuba iliyoko kwenye ncha
ya kusini mwa Bahari ya Chumvi,
3 [k]ukakatiza kusini mwa Akrabimu,
ukaendelea hadi Sini ukaenda hadi
kusini mwa Kadesh-Barnea. Tena
ukapitia Hesroni ukapanda hadi
Adari na ukapinda hadi Karka.
4 [l]Kisha ukaendelea mpaka Azmoni
na kuunganika na Kijito cha Misri, na
kuishia baharini. Huu ndio mpaka wao
wa upande wa kusini.
5 [m]Mpaka wa upande wa mashariki
ni Bahari ya Chumvi ukienea mahali
Mto Yordani unapoingilia.
Mpaka wa upande wa kaskazini
ulianzia penye ghuba ya bahari mahali
Mto Yordani unapoingilia, 6 [n]ukapanda
hadi Beth-Hogla, na kuendelea
kaskazini mwa Beth-Araba hadi kwenye
Jiwe la Bohani mwana wa Reubeni.
7 [o]Kisha mpaka ulipanda hadi Debiri
kutoka Bonde la Akori na kugeuka
kaskazini hadi Gilgali inayotazamana
na materemko ya Adumimu, kusini
mwa bonde. Ukaendelea sambamba
hadi maji ya En-Shemeshi na kutokeza
huko En-Rogeli. 8 [p]Kisha ukapanda
kwa kufuata Bonde la Ben-Hinomu
sambamba na mteremko wa kusini
wa mji mkubwa wa Wayebusi (yaani

[a]**14:8** Hes 13:31; 14:24; 32:12; Kum 1:36; Ufu 14:4
[b]**14:9** Kum 11:24; Hes 14:24; Yos 1:3; Hes 13:22
[c]**14:10** Hes 11:28; 14:30; Yos 5:6; 13:1; Hes 14:30; Kum 31:2; Za 90:10
[d]**14:11** Kum 34:7; Mwa 15:15
[e]**14:12** Hes 14:24-28; 13:33; 1Sam 14:6; 2Nya 14:11, 12; Za 18:32; 44:3; Rum 8:31; Flp 4:13; Yos 15:14; Amu 1:10
[f]**14:13** Yos 22:6-7; 1Sam 30:14; Mwa 23:19; Yos 10:36; Amu 1:26; 1Nya 6:56
[g]**14:14** Hes 14:24
[h]**14:15** Mwa 23:2; Yos 15:13; 11:23; Amu 3:11; 1Fal 4:24; 5:4; 1Nya 22:9
[i]**15:1** Hes 34:3; 13:21; Yos 18:5
[j]**15:2** Mwa 14:3
[k]**15:3** Hes 34:4; Kum 1:2
[l]**15:4** Hes 34:5; Mwa 15:18; 1Fal 8:65
[m]**15:5** Hes 34:10; Mwa 14:3
[n]**15:6** Yos 18:17-21
[o]**15:7** Yos 10:3; 7:24, 26; Kum 11:30; Yos 18:16-17; 2Sam 17:17; 1Fal 1:9; Hos 2:15
[p]**15:8** 2Nya 28:3; Yer 19:6; Yos 18:16, 28; Amu 1:21; 19:10; 2Sam 5:6; 1Nya 11:4; Ezr 9:1; Yos 10:1; 2Fal 23:10; 2Sam 5:18, 22; 1Nya 14:9; Isa 17:5

Yerusalemu). Kutoka hapo ukapanda
juu ya kilima magharibi ya Bonde la
Hinomu mwisho wa ncha ya kaskazini
mwa Bonde la Warefai. [9] [a]Kutoka juu
ya kilima mpaka ule ukaendelea hadi
kwenye chemchemi ya maji ya Neftoa,
ukatokea kwenye miji ya Mlima Efroni
na kuteremka kuelekea Baala (yaani
Kiriath-Yearimu). [10] [b]Kisha ukapinda
upande wa magharibi kutoka Baala
hadi Mlima Seiri, ukafuatia sambamba
mteremko wa kaskazini mwa Mlima
Yearimu (yaani Kesaloni), ukaendelea
chini hadi Beth-Shemeshi na kukatiza
hadi Timna. [11] [c]Ukaelekea hadi kwenye
mteremko wa kaskazini mwa Ekroni,
ukageuka kuelekea Shikeroni, ukapita
hadi Mlima Baala na kufika Yabineeli.
Mpaka ule ukaishia baharini.
[12] [de]Mpaka wa magharibi ni pwani
ya Bahari Kuu.

Hii ndiyo mipaka ya watu wa Yuda kwa
koo zao.

*Nchi Aliyopewa Kalebu*

**(Waamuzi 1:11-15)**

[13] [f]Kwa kufuata maagizo ya BWANA
kwake, Yoshua alimpa Kalebu mwana
wa Yefune sehemu katika Yuda: Kiriath-
Arba, yaani Hebroni (Arba alikuwa baba
wa zamani wa Anaki). [14] [g]Kutoka Hebroni
Kalebu alifukuza hao wana watatu wa
Anaki, nao ni Sheshai, Ahimani na Talmai,
wazao wa Anaki. [15] [h]Kutoka hapo akaondoka
kupigana dhidi ya watu walioishi Debiri
(jina la Debiri hapo kwanza uliitwa Kiriath-
Seferi). [16] [i]Kalebu akasema, "Nitamwoza
binti yangu Aksa kwa mtu atakayeweza
kupigana na kuteka Kiriath-Seferi." [17] [j]Basi
Othnieli mwana wa Kenazi, ndugu yake
Kalebu, akauteka; hivyo Kalebu akamtoa
Aksa binti yake aolewe naye.
[18] [k]Siku moja Aksa alipokuja kwa Othnieli,
alimsihi Othnieli amwombe baba yake,
Kalebu, shamba. Aksa aliposhuka kutoka
juu ya punda wake, Kalebu akamuuliza,
"Je, wataka nikufanyie nini?"
[19] [l]Akamjibu, "Naomba unifanyie jambo
moja la hisani. Kwa kuwa umenipa ardhi
huko Negebu, nipe pia chemchemi za maji."
Basi Kalebu akampa chemchemi za juu na
za chini.

*Miji Ya Yuda*

[20] [m]Huu ndio urithi wa kabila la Yuda,
ukoo kwa ukoo:

[21] [n]Miji ya kusini kabisa ya kabila la Yuda
katika Negebu kuelekea mpaka wa Edomu
ilikuwa:

Kabseeli, Ederi, Yaguri, [22] Kina,
Dimona, Adada, [23] [o]Kedeshi, Hazori,
Ithnani, [24] [p]Zifu, Telemu, Bealothi,
[25] Hazor-Hadata, Kerioth-Hezroni
(yaani Hazori), [26] [q]Amamu, Shema,
Molada, [27] Hasar-Gada, Heshmoni,
Beth-Peleti, [28] [r]Hasar-Shuali, Beer-
Sheba, Biziothia, [29] [s]Baala, Iyimu,
Esemu, [30] [t]Eltoladi, Kesili, Horma,
[31] [u]Siklagi, Madmana, Sansana,
[32] [v]Lebaothi, Shilhimu, Aini na Rimoni;

[a]**15:9** Yos 18:15; 2Sam 6:2; 1Nya 13:9; Yos 9:17
[b]**15:10** Hes 24:18; Yos 19:22; 21:16; Amu 1:33; 1Sam 6:9; 1Fal 4:9; 2Fal 14:11; Mwa 38:12
[c]**15:11** Yos 13:3; 19:43
[d]**15:12** Kum 11:24
[e]**15:12** Hes 34:6
[f]**15:13** 1Sam 25:3; 30:14; Mwa 23:2; Yos 10:36; 21:12; 1Nya 6:56; Hes 13:22
[g]**15:14** Hes 13:33; 13:12; Amu 1:10, 20
[h]**15:15** Yos 10:38
[i]**15:16** 1Nya 2:49; Amu 1:12
[j]**15:17** Amu 3:9; 1Nya 4:13; 27:15; Hes 32:12; Yos 14:6
[k]**15:18** Amu 1:14; Mwa 24:64; 1Sam 25:23
[l]**15:19** Yos 10:40; Mwa 36:24
[m]**15:20** Mwa 49:8-12; Kum 33:7
[n]**15:21** Yos 10:40; 2Sam 23:20; 1Nya 11:22; Mwa 35:21
[o]**15:23** Yos 12:22; 11:1
[p]**15:24** 1Sam 23:14; 2Nya 11:8
[q]**15:26** Yos 19:2; 1Nya 4:28; Neh 11:26
[r]**15:28** Yos 19:3; 1Nya 4:28; Mwa 21:14
[s]**15:29** Yos 19:3; 1Nya 4:29
[t]**15:30** Yos 19:4; Hes 14:45
[u]**15:31** Yos 19:5; 1Nya 4:30; 12:1; Neh 11:28; 1Nya 2:49
[v]**15:32** Hes 34:11; Yos 19:7; Amu 20:45; 21:13; Zek 14:10

hiyo yote ni miji ishirini na tisa,
pamoja na vijiji vyake.

33 [a]Kwenye shefela ya magharibi:
Eshtaoli, Sora, Ashna, 34 [b]Zanoa,
En-Ganimu, Tapua, Enamu,
35 [c]Yarmuthi, Adulamu, Soko, Azeka,
36 [d]Shaaraimu, Adithaimu na Gedera
(au Gederothaimu); yote ni miji kumi
na minne, pamoja na vijiji vyake.
37 Senani, Hadasha, Migdal-Gadi,
38 [e]Dileani, Mispa, Yoktheeli, 39 [f]Lakishi,
Boskathi, Egloni, 40 Kaboni, Lamasi,
Kitlishi, 41 [g]Gederothi, Beth-Dagoni,
Naama na Makeda; yote ni miji kumi
na sita pamoja na vijiji vyake.
42 [h]Libna, Etheri, Ashani, 43 Yifta,
Ashna, Nesibu, 44 [i]Keila, Akzibu na
Maresha; yote ni miji tisa pamoja na
vijiji vyake.
45 [j]Ekroni, pamoja na viunga vyake
na vijiji vyake; 46 [k]magharibi ya Ekroni,
maeneo yote yaliyokuwa karibu
na Ashdodi, pamoja na vijiji vyake;
47 [l]Ashdodi, miji yake na vijiji vyake
na Gaza viunga vyake na vijiji vyake,
hadi kufikia Kijito cha Misri na Pwani
ya Bahari Kuu.

48 [m]Katika nchi ya vilima:
Shamiri, Yatiri, Soko, 49 [n]Dana,
Kiriath-Sana (yaani Debiri), 50 [o]Anabu,
Eshtemoa, Animu, 51 [p]Gosheni, Holoni
na Gilo; miji kumi na mmoja pamoja
na vijiji vyake.
52 [q]Arabu, Duma, Ashani, 53 Yanimu,
Beth-Tapua, Afeka, 54 [r]Humta, Kiriath-
Arba (yaani Hebroni), na Siori; miji
tisa pamoja na vijiji vyake.
55 [s]Maoni, Karmeli, Zifu, Yuta,
56 [t]Yezreeli, Yokdeamu, Zanoa,
57 [u]Kaini, Gibea na Timna; miji kumi
pamoja na vijiji vyake.
58 [v]Halhuli, Beth-Suri, Gedori,
59 Maarathi, Beth-Anothi na Eltekoni;
miji sita pamoja na vijiji vyake.
60 [w]Kiriath-Baali (yaani Kiriath-
Yearimu) na Raba; miji miwili pamoja
na vijiji vyake.

61 [x]Huko jangwani:
Beth-Araba, Midini, Sekaka,
62 [y]Nibshani, Mji wa Chumvi, na
En-Gedi; miji sita pamoja na vijiji
vyake.

63 [z]Yuda hakuweza kuwafukuza Wayebusi,
waliokuwa wakiishi Yerusalemu; hadi leo
Wayebusi huishi huko pamoja na watu wa
Yuda.

---

[a]**15:33** Yos 19:41; Amu 13:25; 16:31; 18:2; 13:2; 18:11; 2Nya 11:10; Neh 11:29
[b]**15:34** Yos 15:34; 1Nya 4:18; Neh 3:13; 11:30; Yos 19:21; 21:29; 12:17
[c]**15:35** Yos 10:3; Mwa 38:1; 1Fal 4:10; Yos 10:10
[d]**15:36** 1Sam 17:52; 1Nya 4:31; 12:4
[e]**15:38** Yos 11:3; 2Fal 14:7
[f]**15:39** Yos 10:3; 2Fal 22:1; 14:19
[g]**15:41** 2Nya 28:18; Yos 19:27; 10:10
[h]**15:42** Hes 33; 20; Yos 19:7; 1Sam 30:30; 1Nya 4:32; 6:59
[i]**15:44** 1Sam 23:1-2; 1Nya 4:19; Neh 3:17-18; Yos 19:29; Amu 1:31; Mik 1:14-15
[j]**15:45** Yos 13:3
[k]**15:46** Yos 11:22
[l]**15:47** Yos 11:22; Mwa 15:18; Hes 34:6
[m]**15:48** Amu 10:1; Yos 21:14; 1Sam 30:27; 1Nya 6:57
[n]**15:49** Yos 10:3
[o]**15:50** Yos 11:21; 21:14; 1Sam 30:28
[p]**15:51** Yos 10:41; 21:15; Yer 48:21; 2Sam 15:12
[q]**15:52** Mwa 25:14
[r]**15:54** Mwa 35:27; Yos 14:15; Amu 1:10
[s]**15:55** Amu 10:12; 1Sam 23:24-25; 25:1-2; 1Nya 2:45; Yos 12:22; 21:16
[t]**15:56** Yos 17:16; 19:18; Amu 6:33; 1Sam 25:43; 1Fal 18:45; 1Nya 3:1; Hos 1:5
[u]**15:57** Yos 18:28; 24:33; Amu 19:12; 20:4; 2Sam 23:29; 1Nya 11:31; Mwa 38:12
[v]**15:58** 1Nya 2:45; 2Nya 11:7; Neh 3:16; 1Nya 4:36; 12:7
[w]**15:60** Yos 9:17; Kum 3:11; Yos 18:14; 1Sam 7:1, 2; 1Nya 13:6
[x]**15:61** Yos 8:15
[y]**15:62** 1Sam 23:29; 24:1; Eze 47:10
[z]**15:63** Yos 16:10; 17:12; Amu 1:21; Yos 10:1; Eze 48:7; Amu 19:10-12; Hes 13:29; 2Sam 14:16, 18; 2Nya 3:1; Zek 9:7

### *Mgawo Kwa Efraimu Na Manase*

16 [a]Mgawanyo wa Yosefu ulianzia
Yordani ya Yeriko, mashariki
mwa miji ya Yeriko na kutoka hapo
ulipanda kupitia jangwani na kuingia
katika nchi ya vilima ya Betheli.
2 [b]Ukaendelea kutoka Betheli (ndiyo
Luzu), ukavuka kuingia eneo la Waariki
huko Atarothi, 3 [c]ukateremkia kuelekea
magharibi hadi eneo la Wayafleti
ukienea hadi eneo la Beth-Horoni ya
Chini hadi Gezeri, ukiishia baharini.
4 [d]Kwa hiyo Manase na Efraimu, wazao wa
Yosefu, walipokea urithi wao.

5 [e]Hili ndilo lilikuwa eneo la Efraimu, ukoo
kwa ukoo:

Mpaka wa urithi wao ulianzia
Ataroth-Adari upande wa mashariki
hadi Beth-Horoni ya Juu, 6 [f]na
kuendelea mpaka baharini. Kutoka
Mikmeta upande wa kaskazini ulipinda
kuelekea mashariki hadi Taanath-
Shilo, ukiupita hadi Yanoa upande wa
mashariki. 7 [g]Kisha uliteremka kutoka
Yanoa hadi Atarothi na Naara, ukagusa
Yeriko na kutokea katika Mto Yordani.
8 [h]Kutoka Tapua mpaka ulikwenda
magharibi hadi Bonde la Kana na
kuishia baharini. Huu ulikuwa ndio
urithi wa kabila la Waefraimu, ukoo
kwa ukoo. 9 [i]Pia ulijumuisha miji yote
na vijiji vyake ambavyo vilitengwa
kwa ajili ya Waefraimu ndani ya urithi
wa kabila la Manase.

10 [j]Hawakuwatoa Wakanaani waishio Gezeri;
mpaka leo Wakanaani wanaishi miongoni
mwa watu wa Efraimu lakini wanatakiwa
kufanya kazi ngumu za kulazimishwa.

### *Mgawo Wa Nusu Nyingine Ya Manase Upande Wa Magharibi*

17 [k]Huu ndio mgawo wa kabila la Manase
kama mzaliwa wa kwanza wa Yosefu,
yaani kwa ajili ya Makiri, mzaliwa wa
kwanza wa Manase. Makiri alikuwa baba
wa Wagileadi, ambao walipokea Gileadi na
Bashani kwa sababu Wamakiri walikuwa
askari wakuu. 2 [l]Kwa hiyo mgawo huu
ulikuwa kwa ajili ya watu wa Manase
waliokuwa wamebaki, ambao ni koo za
Abiezeri, Heleki, Asirieli, Shekemu, Heferi
na Shemida. Hawa ndio wanaume wale
wengine wa uzao wa Manase mwana wa
Yosefu kwa koo zao.

3 [m]Basi Selofehadi mwana wa Heferi,
mwana wa Gileadi, mwana wa Makiri,
mwana wa Manase hakuwa na wana waume
ila mabinti tu, ambao majina yao yalikuwa
Mahla, Noa, Hogla, Milka na Tirsa.
4 [n]Wakamwendea kuhani Eleazari, Yoshua
mwana wa Nuni, na viongozi, wakasema:
"Bwana alimwagiza Mose atupatie urithi
miongoni mwa ndugu zetu." Kwa hiyo
Yoshua akawapa urithi pamoja na ndugu
wa baba yao, kufuatana na agizo la Bwana.
5 [o]Fungu la Manase lilikuwa na sehemu
kumi za nchi, licha ya Gileadi na Bashani
mashariki mwa Yordani, 6 kwa sababu wale
binti za kabila la Manase walipokea urithi
miongoni mwa wana wa kiume. Nchi ya
Gileadi ilikuwa mali ya wazao wa Manase
waliobaki.

7 [p]Eneo la Manase lilienea kuanzia
Asheri hadi Mikmeta mashariki mwa
Shekemu. Mpaka ule ulielekea upande
wa kusini kutoka pale kujumuisha
watu walioishi En-Tapua. 8 [q](Nchi ya
Tapua ilikuwa mali ya Manase, lakini
Tapua yenyewe iliyo mpakani mwa

[a]**16:1** Yos 8:15; 12:9; 18:12
[b]**16:2** Mwa 28:19; 2Sam 15:32; Hes 32:3
[c]**16:3** Yos 10:10; 10:33; 1Fal 9:15
[d]**16:4** Yos 17:14; 18:5
[e]**16:5** Yos 18:13; 10:10
[f]**16:6** Yos 17:7; 2Fal 15:29
[g]**16:7** Hes 32:3
[h]**16:8** Yos 12:17; 17:9; 19:28
[i]**16:9** Eze 48:5
[j]**16:10** Yos 15:63; 17:12-13; Amu 1:28-29; 1Fal 9:16
[k]**17:1** Hes 1:34; 1Nya 7:14; Mwa 41:51; 50:23; Yos 12:2, 5
[l]**17:2** Hes 26:30; Amu 6:11, 34; 8:2; 1Nya 7:14-19; Hes 27:1
[m]**17:3** Hes 27:1; 26:33
[n]**17:4** Hes 27:5-7; Yos 14:1
[o]**17:5** Yos 13:30-31
[p]**17:7** Yos 19:24, 31; 21:6, 30; Amu 1:31; 5:17; 6:35; 7:23; Yos 16:6; Mwa 12:6; Yos 21:12; 24:25
[q]**17:8** Yos 12:17; 15:34

nchi ya Manase ilikuwa ya Waefraimu.)
9 [a]Kisha mpaka ule uliendelea kuelekea
kusini hadi Bonde la Kana. Kulikuwepo
miji ya Efraimu iliyokuwa miongoni
mwa miji ya Manase, lakini mpaka wa
Manase ulikuwa upande wa kaskazini
wa lile bonde na kuishia kwenye
bahari. 10 [b]Nchi ya kusini ilikuwa ya
Efraimu, na ile iliyokuwa upande wa
kaskazini ilikuwa ya Manase. Eneo la
Manase lilifika bahari na ikapakana na
Asheri upande wa kaskazini, na Isakari
upande wa mashariki.
11 [c]Katika Isakari na Asheri Manase
alikuwa na miji pia: Beth-Shani,
Ibleamu na watu wa Dori,[d] Endori,
Taanaki na Megido, pamoja na vijiji
vyote vinavyohusika na miji hiyo (ya
tatu katika orodha ni Nafothi).
12 [e]Lakini Wamanase hawakuweza kuimiliki
miji hii, kwa kuwa Wakanaani walikazana
kuishi katika maeneo hayo. 13 [f]Hata hivyo,
Waisraeli walivyoendelea kupata nguvu
waliwatumikisha Wakanaani na kuwatia
katika kazi za kulazimishwa, lakini
hawakuwafukuza kabisa.

### *Kabila La Yosefu Lakataa*

14 [g]Watu wa Yosefu wakamwambia
Yoshua, "Kwa nini umetupa sisi mgawo
mmoja tu na sehemu moja tu kuwa
urithi? Sisi tu watu wengi sana, na Bwana
ametubariki kwa wingi."
15 [h]Yoshua akajibu, "Kama ninyi ni wengi
sana, na kama nchi ya vilima ya Efraimu
ni ndogo sana kwenu, pandeni msituni
mkafyeke eneo kwa ajili yenu wenyewe
huko kwenye nchi ya Waperizi na Warefai."
16 [i]Watu wa Yosefu wakajibu, "Hiyo nchi
ya vilima haitutoshi, nao Wakanaani wote
wanaoishi katika tambarare wanayo magari
ya vita ya chuma, wote wa Beth-Shani na
miji yake, na wale walio katika Bonde la
Yezreeli."
17 [j]Lakini Yoshua akanena na nyumba ya
Yosefu, yaani Efraimu na Manase: "Ninyi
ni wengi sana na wenye nguvu sana.
Hamtakuwa na mgawo mmoja tu, 18 [k]bali
pia nchi hii ya kilima yenye msitu. Ifyekeni,
nayo mipaka yake itakuwa yenu umbali
mtakaoweza kufika. Ingawa Wakanaani
wana magari ya chuma, nao wana nguvu,
mwaweza kuwafukuza humo."

### *Mgawanyo Wa Nchi Iliyobaki*

18 [l]Kusanyiko lote la Waisraeli
likakusanyika huko Shilo na
kusimamisha Hema la Kukutania. Nchi
ikawa chini ya utawala wao, 2 lakini
palikuwa bado makabila saba ya Israeli
ambayo yalikuwa hayajapokea urithi wao.
3 [m]Hivyo Yoshua akawaambia Waisraeli,
"Je, mtasubiri hata lini ili kuingia
kumiliki nchi ambayo Bwana, Mungu
wa baba zenu, amewapa? 4 [n]Chagueni
watu watatu kutoka kwenye kila kabila.
Nitawatuma hao watu kukagua hiyo nchi
na kuniandikia mapendekezo ya mgawanyo
wa urithi wa kila kabila. Nao watanirudia.
5 [o]Mtaigawanya hiyo nchi katika sehemu
saba. Yuda atabaki katika eneo lake upande
wa kusini na nyumba ya Yosefu katika nchi
yake upande wa kaskazini. 6 [p]Baada ya
kuandika maelezo ya hizo sehemu saba za

[a]**17:9** Yos 16:8
[b]**17:10** Mwa 30:18; Eze 48:5
[c]**17:11** Amu 1:27; 1Sam 31:10; 2Sam 21:12; 1Fal 4:12; 1Nya 7:29; 2Fal 9:27; Yos 11:2; 1Sam 28:7; Za 83:10; Yos 12:21; 1Fal 9:15; Eze 48:4
[d]11 Ndiyo Nafoth-Dori.
[e]**17:12** Yos 15:63; Hes 26:29; 32:39, 41
[f]**17:13** Amu 1:27-28; Kut 23:29-33; Amu 1:27, 28
[g]**17:14** Hes 26:28-37; Yos 16:4; Mwa 48:22; 48:19
[h]**17:15** 2Sam 18:6; Yos 3:10; Mwa 14:5; Yos 15:8; 18:16; 2Sam 5:18; 23:13; 1Sam 17:5
[i]**17:16** Amu 1:19; 4:3, 13; Yos 15:56; 1Sam 29:1; Amu 6:33; 1Fal 4:12; 18:46
[j]**17:17** Eze 48:5
[k]**17:18** 1Sam 1:1; Kum 20:1; Yos 11:4-6; 13:6; Rum 8:31; Ebr 13:6
[l]**18:1** Yos 19:51; 21:2; Amu 18:31; 21:12; 1Sam 1:3; 3:21; 4:3; 1Fal 14:2; Za 78:60; Yer 7:12; 26:6; 41:5; Kut 27:21; 40:2; Mdo 7:45
[m]**18:3** Amu 18:9; Sef 3:16; Mt 20:6; Yn 6:27; Flp 3:13-14
[n]**18:4** Mik 2:5
[o]**18:5** Yos 15:1; 16:1-4
[p]**18:6** Law 16:8; Yos 14:2

nchi, yaleteni kwangu, nami nitawapigia
kura kwa kura mbele za BWANA Mungu
wetu. 7 [a]Hata hivyo, Walawi hawatakuwa
na sehemu miongoni mwenu, kwa maana
huduma ya ukuhani kwa BWANA ndio urithi
wao. Nao Gadi, Reubeni na nusu ya kabila
la Manase wameshapata urithi wao upande
wa mashariki mwa Yordani, ambako Mose
mtumishi wa BWANA aliwapa."

8 Watu hao walipokuwa wanaondoka
kwenda kuandika vizuri kuhusu hiyo nchi,
Yoshua akawaagiza, "Nendeni mkakague
hiyo nchi na mwandike maelezo kuihusu.
Kisha mrudi kwangu, nami nitawapigia
kura hapa Shilo mbele za BWANA." 9 Ndipo
hao watu walipoondoka na kupita katika
ile nchi. Wakaandika maelezo yake kwenye
kitabu, mji kwa mji, katika sehemu saba
na kurudisha taarifa kwa Yoshua huko
kambini Shilo. 10 [b]Basi Yoshua akawapigia
kura huko Shilo mbele za BWANA, na
hapo akagawanya ile nchi kwa Waisraeli
kufuatana na mgawanyo wa kabila zao.

*Mgawo Kwa Benyamini*

11 Kura iliangukia kabila la Benyamini, ukoo
kwa ukoo. Eneo lao walilogawiwa lilikuwa
kati ya kabila la Yuda na la Yosefu.

12 [c]Upande wa kaskazini mpaka
wao ulianzia pale Yordani, kupitia
kaskazini ya mteremko wa Yeriko na
kuendelea magharibi kuingia katika
nchi ya vilima, ukitokea kwenye
jangwa la Beth-Aveni. 13 [d]Kutoka hapo
ulikatiza kwenye mteremko wa kusini
mwa Luzu (yaani Betheli) na kushuka
hadi Ataroth-Adari katika kilima kusini
mwa Beth-Horoni ya Chini.

14 [e]Kutoka kilima kinachotazamana
na Beth-Horoni upande wa kusini
mpaka ule ukazunguka kusini kufuatia
upande wa magharibi, na ukatokezea
Kiriath-Baali (yaani Kiriath-Yearimu),
mji wa watu wa Yuda. Huu ndio
uliokuwa upande wa magharibi.

15 [f]Upande wa kusini mpaka ulianzia
kwenye viunga vya Kiriath-Yearimu
kwa upande wa magharibi, nao
ukatokeza kwenye chemchemi ya
maji ya Neftoa. 16 [g]Mpaka ukateremka
hadi shefela inayotazamana na Bonde
la Ben-Hinomu, kaskazini mwa
Bonde la Refaimu. Ukaendelea chini
kwenye Bonde la Hinomu sambamba
na mteremko wa kusini mwa mji
mkubwa wa Wayebusi na kisha
hadi En-Rogeli. 17 [h]Kisha ukapinda
kuelekea kaskazini, ukaenda hadi
En-Shemeshi na kuendelea mpaka
Gelilothi, inayotazamana na Njia ya
Adumimu, ukateremka hadi kwenye
Jiwe la Bohani mwana wa Reubeni.
18 [i]Ukaendelea upande wa mteremko wa
kaskazini wa Beth-Araba ukateremka
hadi Araba. 19 [j]Kisha ukaenda mpaka
kwenye mteremko wa kaskazini wa
Beth-Hogla na kujitokeza kwenye
ghuba ya kaskazini ya Bahari ya
Chumvi, kwenye maingilio ya Yordani
upande wa kusini. Huo ulikuwa mpaka
wa kusini.

20 [k]Nayo Yordani ikawa ndio mpaka
wa upande wa mashariki.

Hii ilikuwa ndiyo mipaka iliyoonyesha
urithi wa koo za Benyamini pande zote.

21 [l]Kabila ya Benyamini, ukoo kwa ukoo,
ilikuwa na miji mikubwa ifuatayo:

Yeriko, Beth-Hogla, Emeki-Kesisi,
22 [m]Beth-Araba, Semaraimu, Betheli,

---

[a]**18:7** Yos 13:33; 13:8
[b]**18:10** Hes 34:13; Yer 7:12; Hes 33:54; Yos 19:51; Mit 16:33
[c]**18:12** Yos 8:15; 7:2
[d]**18:13** Mwa 28:19; Yos 12:9; Hes 32:3; Yos 16:5; Amu 1:23; Hes 18:20; Kum 10:9; Eze 44:28
[e]**18:14** Yos 10:10; 9:17; 1Nya 13:6
[f]**18:15** Yos 15:9
[g]**18:16** Yos 17:15; 15:7-8; 2Fal 23:10; 2Nya 28:3; 33:6; Isa 30:33; Yer 19:2; Yos 15:8
[h]**18:17** Yos 22:10; 15:6-7
[i]**18:18** Yos 15:6; 11:2; 16:1
[j]**18:19** Yos 15:6; Mwa 14:3
[k]**18:20** 1Sam 9:1; Yos 21:4, 17
[l]**18:21** Yos 6:26; 1Fal 16:34; Lk 10:30
[m]**18:22** Yos 15:6; 2Nya 13:4; Yos 16:1

23 [a]Avimu, Para na Ofra, 24 [b]Kefar-
Amoni, Ofni, na Geba; miji kumi na
miwili pamoja na vijiji vyake.
25 [c]Gibeoni, Rama na Beerothi,
26 [d]Mispa, Kefira, Moza, 27 Rekemu,
Irpeeli, Tarala, 28 [e]Zela, Elefu, mji wa
Wayebusi (yaani Yerusalemu), Gibea
na Kiriathi; miji kumi na minne pamoja
na vijiji vyake.

Huu ndio uliokuwa urithi wa Benyamini kwa ajili ya koo zake.

*Mgawo Kwa Simeoni*

19 [f]Kura ya pili ikaangukia kabila la
Simeoni, ukoo kwa ukoo. Urithi
wao ulikuwa ndani ya eneo la Yuda.
2 [g]Ulijumuisha:

Beer-Sheba (au Sheba), Molada,
3 [h]Hasar-Shuali, Bala, Esemu,
4 Eltoladi, Bethuli, Horma, 5 Siklagi,
Beth-Markabothi, Hasar-Susa, 6 Beth-
Lebaothi na Sharuheni; hii ilikuwa miji
kumi na mitatu pamoja na vijiji vyake.
7 Pia Aini, Rimoni, Etheri, na
Ashani; hii ilikuwa miji minne na
vijiji vyake, 8 pamoja na vijiji vyote
vinavyoizunguka miji hii mpaka
Baalath-Beeri (ambayo ndiyo Rama
iliyo katika Negebu).

Huu ulikuwa ni urithi wa kabila la Simeoni
ukoo kwa ukoo. 9 [i]Urithi wa Wasimeoni
ulitolewa kutoka fungu la Yuda, kwa
kuwa fungu la Yuda lilikuwa kubwa kuliko
walivyohitaji. Hivyo kabila la Simeoni
lilipewa urithi wao ndani ya eneo la Yuda.

*Mgawo Kwa Zabuloni*

10 [j]Kura ya tatu ikaangukia kabila la
Zabuloni, ukoo kwa ukoo:

Mpaka wa urithi wao uliendelea
hadi Saridi. 11 [k]Kuelekea upande wa
magharibi ukafika Marala, ukagusa
Dabeshethi, na kuendelea mpaka
kwenye bonde karibu na Yokneamu.
12 [l]Ukageuka mashariki, kuanzia
Saridi kuelekea mawio ya jua hadi
kwenye nchi ya Kisiloth-Tabori, na
kwenda hadi Daberathi, kupanda
Yafia. 13 Kisha ukaendelea mashariki
hadi Gath-Heferi na kufika Eth-Kasini,
ukatokea Rimoni na kugeuka kuelekea
Nea. 14 [m]Huko mpaka ukazungukia
upande wa kaskazini hadi Hanathoni
na kuishia katika Bonde la Ifta-Eli.
15 [n]Miji mingine iliyojumuishwa ni
Katathi, Nahalali, Shimroni, Idala na
Bethlehemu. Kulikuwa na miji kumi na
miwili pamoja na vijiji vyake.

16 [o]Miji hii na vijiji vyake ilikuwa ndio urithi
wa Zabuloni, ukoo kwa ukoo.

*Mgawo Kwa Isakari*

17 [p]Kura ya nne ikamwangukia Isakari, ukoo
kwa ukoo. 18 [q]Eneo lao lilijumuisha:

Yezreeli, Kesulothi, Shunemu,
19 Hafaraimu, Shioni, Anaharathi,
20 [r]Rabithi, Kishioni, Ebesi, 21 [s]Remethi,
En-Ganimu, En-Hada na Beth-Pasesi.
22 [t]Mpaka ule ukagusa Tabori,
Shahasuma na Beth-Shemeshi, na
ukaishia kwenye Yordani. Ilikuwa miji
kumi na sita, pamoja na vijiji vyake.

---

[a]**18:23** Kum 2:23; Amu 6:11, 24; 8:27, 32; 9:6; 1Sam 13:17
[b]**18:24** Yos 21:17; 1Sam 13:3, 16; 14:5; 1Fal 15:22; 2Fal 23:8; Isa 10:29; Amu 19:12-16; Ezr 2:26
[c]**18:25** Yos 10:40; Amu 4:5; 19:13; 1Sam 2:11; 7:17; 25:1; Neh 11:33; 1Fal 15:17, 21; Neh 7:29
[d]**18:26** Yer 11:3; Yos 9:17; Ezr 2:25; Neh 7:29
[e]**18:28** 2Sam 21:14; Yos 15:8; 10:1; 15:57; 9:17; Eze 48:23; Mwa 46:21; Mdo 17:26
[f]**19:1** Mwa 49:7
[g]**19:2** Mwa 21:14; 1Fal 19:3; Yos 15:26; 1Nya 4:28; Neh 11:26
[h]**19:3** Yos 15:28-29
[i]**19:9** Mwa 47:9; Eze 48:24
[j]**19:10** Yos 21:7, 34
[k]**19:11** Yos 12:22
[l]**19:12** Yos 22; 21:28; 1Nya 6:72
[m]**19:14** Mwa 49:13; Hes 34:6-7; Kut 23:31; 1Fal 4:12
[n]**19:15** Yos 21:35; 11:1; Mwa 35:19; Amu 1:30
[o]**19:16** Eze 48:26; Yos 21:7; Mdo 17:26
[p]**19:17** Mwa 30:18
[q]**19:18** Yos 15:56; Isa 28:4; 1Fal 1:3; 2Fal 4:8
[r]**19:20** Yos 21:28
[s]**19:21** Yos 15:34
[t]**19:22** Amu 4:6, 12; 8:18; Za 89:12; Yer 46:18; Yos 15:10

23 [a]Miji hii pamoja na vijiji vyake ilikuwa
urithi wa kabila la Isakari, ukoo kwa ukoo.

*Mgawo Kwa Asheri*

24 [b]Kura ya tano ikaangukia kabila la Asheri,
ukoo kwa ukoo. 25 [c]Eneo lao lilijumuisha:
Helkathi, Hali, Beteni, Akishafu,
26 [d]Alameleki, Amadi na Mishali.
Upande wa magharibi mpaka uligusa
Karmeli na Shihor-Libnathi. 27 [e]Tena
ukageuka mashariki kuelekea Beth-
Dagoni, ukagusa Zabuloni na Bonde
la Ifta-Eli, ukaenda upande wa
kaskazini hadi Beth-Emeki na Neyeli,
ukipitia Kabul upande wa kushoto.
28 [f]Ukaendelea hadi Abdoni, Rehobu,
Hamoni na Kana, na kufika Sidoni
Kuu. 29 [g]Mpaka huo ukageukia nyuma
kuelekea Rama na kwenda hadi kwenye
mji wenye ngome wa Tiro, ukageuka
kuelekea Hosa na kutokeza baharini
katika eneo la Akzibu, 30 [h]Uma, Afeki
na Rehobu. Ilikuwepo miji ishirini na
miwili, pamoja na vijiji vyake.
31 [i]Miji hii pamoja na vijiji vyake ilikuwa
ndio urithi wa kabila la Asheri, ukoo kwa
ukoo.

*Mgawo Kwa Naftali*

32 Kura ya sita ikaangukia kabila la Naftali,
ukoo kwa ukoo:
33 [j]Mpaka wao uliendelea kutoka
Helefi na kwenye mti mkubwa ulio
katika Saananimu, ukipitia Adami-
Nekebu na Yabineeli hadi Lakumu,
na kuishia katika Mto Yordani.
34 [k]Mpaka ukaendelea magharibi
kupitia Aznoth-Tabori na kutokea
Hukoki. Ukagusa Zabuloni upande wa
kusini, Asheri upande wa magharibi,
na Yordani upande wa mashariki.
35 [l]Miji yenye ngome ilikuwa Sidimu,
Seri, Hamathi, Rakathi, Kinerethi,
36 [m]Adama, Rama, Hazori, 37 [n]Kedeshi,
Edrei, na En-Hasori, 38 [o]Ironi, Migdal-
Eli, Horemu, Beth-Anathi na Beth-
Shemeshi. Kulikuwa na miji kumi na
tisa na vijiji vyake.
39 [p]Miji hiyo pamoja na vijiji vyake ndio
iliyokuwa urithi wa kabila la Naftali, ukoo
kwa ukoo.

*Mgawo Kwa Dani*

40 Kura ya saba ikaangukia kabila la Dani,
ukoo kwa ukoo. 41 [q]Eneo la urithi wao
lilijumuisha:
Sora, Eshtaoli, Iri-Shemeshi,
42 [r]Shaalabini, Aiyaloni, Ithla, 43 [s]Eloni,
Timna, Ekroni, 44 [t]Elteke, Gibethoni,
Baalathi, 45 [u]Yehudi, Bene-Beraki, Gath-
Rimoni, 46 [v]Me-Yarkoni na Rakoni,
pamoja na eneo linalotazamana na
Yafa.
47 [w](Lakini Wadani walipata shida
kulimiliki eneo lao; kwa hiyo walipanda
kuishambulia Leshemu, wakaitwaa,
wakawaua watu wake kwa upanga na
kuukalia. Walikaa Leshemu na kuuita Dani
kufuatana na jina la baba yao.)

---

[a]**19:23** Yos 17:10; Mwa 49:15; Eze 48:25
[b]**19:24** Yos 17:7
[c]**19:25** Yos 11:1; 1Sam 2:16
[d]**19:26** Yos 21:30; 12:22; 1Fal 18:19; 2Fal 2:25
[e]**19:27** Yos 15:41
[f]**19:28** Yos 21:30; 1Nya 6:74; Hes 13:21; Amu 1:31; 1Nya 6:76; Yos 16:8; Mwa 10:16-19; Yos 11:8
[g]**19:29** Yos 18:25; 2Sam 5:11; 24:7; Ezr 3:7; Za 45:12; Isa 23:1; Yer 25:22; Eze 26:2; Amu 5:17; Yos 15:44; Amu 1:31
[h]**19:30** Yos 12:18
[i]**19:31** Mwa 30:13; Yos 17:7; Eze 48:2
[j]**19:33** Amu 4:11; Yos 15:11
[k]**19:34** 1Nya 6:75; Kum 33:23
[l]**19:35** 1Nya 2:55; Yos 11:2; Hes 13:21; 1Fal 14:25; Yer 39:5; Mk 6:53
[m]**19:36** Yos 18:25; 11:1
[n]**19:37** Yos 12:22; Hes 21:33
[o]**19:38** Amu 1:33; Yos 15:10
[p]**19:39** Kum 33:23; Eze 48:3
[q]**19:41** Yos 15:33; Amu 13:2
[r]**19:42** Amu 1:35; Yos 10:12; 1Fal 4:9
[s]**19:43** Mwa 38:12; Yos 13:3
[t]**19:44** Yos 21:23; 1Fal 15:27; 16:15; 9:18; 2Nya 8:6
[u]**19:45** Yos 21:24; 1Nya 6:69
[v]**19:46** 2Nya 2:16; Ezr 3:7; Yon 1:3; Mdo 9:36
[w]**19:47** Amu 18:1, 7, 14; Kum 3:14; Amu 18:27-29; Mwa 49:17

48 [a]Miji hii na vijiji vyake ndio iliyokuwa
urithi wa kabila la Dani, ukoo kwa ukoo.

*Mgawo Kwa Yoshua*

49 Walipomaliza kugawanya nchi
katika migawo kulingana na sehemu zao
zilizowaangukia, Waisraeli wakampa
Yoshua mwana wa Nuni urithi katikati
yao, 50 [b]kama vile BWANA alivyokuwa
ameamuru. Walimpa mji alioutaka, ambao
ni Timnath-Sera[c] ulio katika nchi ya vilima
ya Efraimu. Naye akajenga mji, akakaa
huko.

51 [d]Haya ndiyo maeneo ambayo kuhani
Eleazari, Yoshua mwana wa Nuni, na
viongozi wa koo za kabila za Israeli
waliyoyagawanya kwa kura huko Shilo
mbele za BWANA penye ingilio la Hema la
Kukutania. Hivyo wakamaliza kuigawanya
nchi.

*Miji Ya Makimbilio*

**(Hesabu 35:9-34)**

20 Ndipo BWANA akamwambia Yoshua,
2 [e]"Waambie Waisraeli, watenge
miji mikubwa ya kukimbilia, kama
nilivyokuagiza kupitia Mose, 3 [f]ili mtu
yeyote atakayemuua mtu kwa bahati mbaya
na pasipo kukusudia aweze kukimbilia huko
na kujiepusha na mlipiza kisasi wa damu.
4 [g]"Anapokimbilia mojawapo ya hii miji
mikubwa atasimama kwenye maingilio ya
lango la mji mkuu na kueleza wazee wa
mji kuhusu shauri lake. Kisha watampokea
katika mji wao na kumpa mahali pa
kuishi nao. 5 [h]Kama mlipiza kisasi wa
damu akimfuatilia, wasimkabidhi yule
mshtakiwa, kwa sababu alimuua jirani
yake bila kukusudia, na bila kuwa na nia
ya kudhuru. 6 [i]Huyu aliyeua atakaa kwenye
mji mkubwa huo mpaka awe amesimama
kukabili mashtaka yake mbele ya kusanyiko
na mpaka kuhani mkuu anayehudumu
kwa wakati huo atakapokufa. Ndipo
atakapoweza kurudi nyumbani kwake
katika mji ambao aliukimbia."

7 [j]Basi wakatenga Kedeshi katika Galilaya
kwenye nchi ya vilima ya Naftali, Shekemu
katika nchi ya vilima ya Efraimu, na Kiriath-
Arba (yaani Hebroni) kwenye nchi ya vilima
ya Yuda. 8 [k]Katika upande wa mashariki
mwa Yordani ya Yeriko wakatenga Bezeri
katika jangwa katika uwanda wa juu
katika kabila la Reubeni, Ramothi katika
Gileadi katika kabila la Gadi, na Golani
huko Bashani katika kabila la Manase.
9 [l]Mwisraeli yeyote au mgeni yeyote aishiye
miongoni mwao aliyemuua mtu kwa bahati
mbaya, angeweza kukimbilia katika miji
mikubwa hiyo iliyotengwa na asiuawe na
mlipiza kisasi wa damu kabla hajasimama
kukabili mashtaka mbele ya kusanyiko.

*Miji Kwa Walawi*

21 [m]Basi viongozi wa jamaa ya Walawi,
wakamwendea kuhani Eleazari,
Yoshua mwana wa Nuni, na viongozi wa
jamaa nyingine za makabila ya Israeli
2 [n]huko Shilo katika Kanaani na kuwaambia,
"BWANA aliamuru kupitia Mose kuwa mtupe
miji ya kuishi yenye sehemu za malisho kwa
mifugo yetu." 3 Hivyo kama vile BWANA
alivyoamuru, Waisraeli wakawapa Walawi
miji ifuatayo pamoja na sehemu zake za
malisho kutoka urithi wao wenyewe.
4 Kura ya kwanza ikaangukia Wakohathi,
ukoo kwa ukoo. Walawi waliokuwa wazao
wa kuhani Aroni walipewa miji kumi na
mitatu kutoka makabila ya Yuda, Simeoni
na Benyamini. 5 Wazao wengine waliobaki

---

[a]**19:48** Mwa 30:6; Hes 26:54; Mdo 17:26
[b]**19:50** Yos 24:30; Amu 2:9
[c]50 Unajulikana pia kama Timnath-Heresi, ona Yos 24:30; Amu 2:9.
[d]**19:51** Yos 23:4; 14:1; 18:10; Mdo 13:19; Hes 34:17; Amu 21:19; Za 78:58
[e]**20:2** Kut 21:13; Hes 35:6-14; Kum 4:41-43; Ebr 6:18-19
[f]**20:3** Law 4:2; Hes 35:12
[g]**20:4** Mwa 23:10; Rut 4:1; Yer 35:7; Yos 7:6
[h]**20:5** 2Nya 10:1; Lk 1:39
[i]**20:6** Hes 35:12
[j]**20:7** Yos 12:22; Mwa 12:6; 35:27; Yos 10:36; Lk 1:36; Yos 21:11, 32; 1Nya 6:76
[k]**20:8** Yos 21:36; 1Nya 6:78-80; Yos 12:2-5; 1Nya 6:71
[l]**20:9** Law 4:2; Kut 21:13; Hes 35:13
[m]**21:1** Yos 14:1; Hes 34:17; Yos 17:4; 24:33
[n]**21:2** Yos 18:1; Hes 35:2-3; Law 25:2; Yos 14:4

wa Wakohathi walipewa miji kumi kutoka
koo za makabila ya Efraimu, Dani na nusu
ya Manase.
6 [a]Wazao wa Gershoni walipewa miji
kumi na mitatu kutoka koo za makabila ya
Isakari, Asheri, Naftali na nusu ya Manase
huko Bashani.
7 [b]Wazao wa Merari, ukoo kwa ukoo,
walipewa miji kumi na miwili kutoka
makabila ya Reubeni, Gadi na Zabuloni.
8 [c]Kwa hiyo Waisraeli wakawapa Walawi
miji hii pamoja na sehemu zake za malisho,
kama vile BWANA alivyokuwa ameamuru
kupitia kwa Mose.

9 Kutoka makabila ya Yuda na Simeoni
waligawa miji ifuatayo kwa majina
10 (miji hii walipewa wazao wa Aroni
ambao walitokana na koo za Wakohathi
wa Walawi, kwa sababu kura ya kwanza
iliwaangukia):

11 [d]Waliwapa Kiriath-Arba (yaani
Hebroni), pamoja na sehemu zake za
malisho zilizoizunguka, katika nchi ya
vilima ya Yuda. (Arba alikuwa baba wa
Anaki.) 12 [e]Lakini mashamba na vijiji
vilivyozunguka mji mkubwa walikuwa
wamempa Kalebu mwana wa Yefune
kuwa milki yake.
13 [f]Kwa hiyo wazao wa kuhani
Aroni wakapewa Hebroni (mji mkuu
wa makimbilio kwa ajili ya yeyote
aliyeshtakiwa kwa mauaji), Libna,
14 [g]Yatiri, Eshtemoa, 15 Holoni, Debiri,
16 [h]Aini, Yuta na Beth-Shemeshi,
pamoja na sehemu zake za malisho,
ilikuwa miji tisa kutoka kwa makabila
haya mawili.
17 [i]Kutoka kabila la Benyamini
wakawapa Gibeoni, Geba, 18 [j]Anathothi
na Almoni, pamoja na sehemu zake za
malisho, ilikuwa miji minne.
19 [k]Miji yote waliyopewa makuhani, wazao
wa Aroni, ilikuwa kumi na mitatu, pamoja
na sehemu zake za malisho.

20 Koo nyingine za Wakohathi, ambao pia
ni Walawi, walipewa miji kutoka kabila
la Efraimu:

21 [l]Katika nchi ya vilima ya Efraimu
walipewa Shekemu (mji mkubwa wa
makimbilio kwa yeyote anayeshtakiwa
kwa mauaji) na Gezeri, 22 [m]Kibsaimu na
Beth-Horoni, pamoja na sehemu zake
za malisho, ilikuwa miji minne.
23 [n]Pia kutoka kabila la Dani
wakapokea Elteke, Gibethoni,
24 [o]Aiyaloni na Gath-Rimoni pamoja
na sehemu zake za malisho, ilikuwa
miji minne
25 [p]Kutoka nusu ya kabila la Manase,
wakapokea Taanaki na Gath-Rimoni
pamoja na sehemu zake za malisho,
ilikuwa miji miwili.

26 Miji yote hii kumi pamoja na sehemu
zake za malisho ilipewa koo za Wakohathi
zilizobaki.

27 [q]Koo za Walawi za Wagershoni walipewa:

kutoka nusu ya kabila la Manase,
Golani katika Bashani (mji mkuu
wa makimbilio kwa yeyote
aliyeshtakiwa kwa mauaji) na
Beeshtera, pamoja na sehemu zake
za malisho, ilikuwa miji miwili;
28 [r]kutoka kabila la Isakari walipewa,

---

[a]**21:6** Hes 3:17; Mwa 30:18; Yos 17:7
[b]**21:7** Kut 6:16; Yos 19:10
[c]**21:8** Mwa 49:7; Hes 35:2-3; Yos 18:6; Mit 16:33
[d]**21:11** Yos 15:48-50
[e]**21:12** Yos 15:13
[f]**21:13** Hes 35:6; 33:20; 1Nya 6:57
[g]**21:14** Yos 15:48-50; Kum 4:43; 1Fal 22:3
[h]**21:16** Hes 34:11; Yos 15:55; 15:10
[i]**21:17** Yos 9:3; Neh 11:31; 1Nya 6:55; Mwa 23:2; Yos 14:15; 2Sam 2:1-3; Lk 1:39
[j]**21:18** 2Sam 23:27; 1Fal 2:26; Ezr 2:23; Neh 7:27; 11:32; Isa 10:30; Yer 1:1; 11:21; 32:7; Yos 14:14
[k]**21:19** 2Nya 31:15; Yos 20:7-9; 15:54; Isa 37:8
[l]**21:21** Yos 17:7; 10:33; 20:7; Mwa 33:19; Amu 9:1; 1Fal 12:1
[m]**21:22** Yos 10:10; 1Sam 1:1
[n]**21:23** Yos 19:44
[o]**21:24** Yos 10:12; 19:45
[p]**21:25** Yos 12:21
[q]**21:27** Yos 12:5; Hes 35:6; Kum 4:43; 1Nya 6:71-76
[r]**21:28** Mwa 30:18; Yos 19:20; 19:12

Kishioni, Daberathi, 29 [a]Yarmuthi na
En-Ganimu, pamoja na sehemu zake
za malisho, ilikuwa miji minne
30 [b]kutoka kabila la Asheri walipewa,
Mishali, Abdoni, 31 [c]Helkathi na
Rehobu, pamoja na sehemu zake za
malisho, ilikuwa miji minne.
32 [d]Kutoka kabila la Naftali walipewa,
Kedeshi katika Galilaya (mji wa
makimbilio kwa ajili ya yeyote
anayeshtakiwa kwa mauaji),
Hamoth-Dori na Kartani, pamoja
na sehemu zake za malisho, ilikuwa
miji mitano.

33 Miji yote ya koo za Wagershoni ilikuwa
kumi na mitatu, pamoja na sehemu zake
za malisho.

34 [e]Koo za Wamerari (Walawi waliobaki)
walipewa:

kutoka kabila la Zabuloni,
Yokneamu, Karta, 35 [f]Dimna na
Nahalali, pamoja na sehemu zake za
malisho, ilikuwa miji minne;
36 [g]kutoka kabila la Reubeni walipewa
Bezeri, Yahasa, 37 [h]Kedemothi na
Mefaathi, pamoja na sehemu zake za
malisho, ilikuwa miji minne;
38 [i]kutoka kabila la Gadi walipewa,
Ramothi katika Gileadi (mji wa
makimbilio kwa ajili ya yeyote
anayeshtakiwa kwa ajili ya mauaji),
Mahanaimu, 39 [j]Heshboni na Yazeri,
pamoja na sehemu zake za malisho,
ilikuwa miji minne.

40 Miji yote waliyopewa koo za Wamerari,
waliokuwa mabaki ya Walawi, ilikuwa ni
kumi na miwili.

41 [k]Miji yote ya Walawi katika eneo
lililoshikwa na Waisraeli lilikuwa arobaini
na minane, pamoja na sehemu zake za
malisho. 42 Kila mmoja wa miji hii ulikuwa
na sehemu ya malisho kuuzunguka; ndivyo
ilivyokuwa kwa miji hii yote.

43 [l]Kwa hiyo Bwana akawapa Israeli
nchi yote aliyokuwa ameapa kuwapa
baba zao, nao wakaimiliki na kukaa humo.
44 [m]Bwana akawapa pumziko kila upande,
kama vile alivyokuwa amewaapia baba zao,
hakuna hata mmoja wa adui zao aliyeweza
kusimama mbele yao, Bwana akawatia
adui zao wote mikononi mwao. 45 [n]Hakuna
hata mojawapo ya ahadi nzuri ya Bwana
kwa nyumba ya Israeli ambayo haikutimia;
kila moja ilitimia.

### *Makabila Ya Mashariki Yarudi Nyumbani*

22 [o]Ndipo Yoshua akawaita Wareubeni,
Wagadi na nusu ya kabila la Manase,
2 [p]naye akawaambia, "Mmeshafanya
yale yote Mose mtumishi wa Bwana
aliyowaamuru, nanyi mmenitii kwa kila
jambo nililowaamuru. 3 Kwa muda mrefu
sasa, hadi siku hii ya leo, hamkuwaacha
ndugu zenu, bali ninyi mmetimiza ile kazi
Bwana Mungu wenu aliyowapa. 4 [q]Sasa
kwa kuwa Bwana Mungu wenu amewapa
ndugu zenu pumziko kama alivyoahidi,
rudini nyumbani mwenu katika nchi
ile ambayo Mose mtumishi wa Bwana
aliwapa ng'ambo ya Yordani. 5 [r]Lakini mwe
waangalifu sana kushika amri na sheria
zile Mose mtumishi wa Bwana alizowapa:
yaani kumpenda Bwana Mungu wenu na
kuenenda katika njia zake zote, kutii amri
zake, kushikamana naye kwa uthabiti na

[a]**21:29** Yos 10:3; 15:34
[b]**21:30** Yos 17:7; 19:26-28
[c]**21:31** Yos 19:28
[d]**21:32** Yos 12:22; Hes 35:6; Yos 12:22
[e]**21:34** Yos 19:10; 12:22
[f]**21:35** Yos 19:15
[g]**21:36** Yos 20:8; Hes 21:23; Kum 2:32; Amu 11:20
[h]**21:37** Yos 13:18
[i]**21:38** Kum 4:43; Yos 12:2; Mwa 32:2
[j]**21:39** Yos 13:25
[k]**21:41** Hes 35:7; Mwa 49:7; Kum 33:10
[l]**21:43** Kum 34:4; 11:31; 17:14
[m]**21:44** Kut 33:14; Kum 6:19; Kut 23:31; Kum 21:10; 7:24
[n]**21:45** Yos 23:14; Neh 9:8; Isa 49:7-8; Mt 24:35; Lk 21:33
[o]**22:1** Hes 32:25
[p]**22:2** Kum 3:18; Hes 32:20
[q]**22:4** Kut 33:14; Hes 32:22; Kum 3:22; Hes 32:18; Yos 1:13-15
[r]**22:5** Isa 43:22; Mal 3:14; Yos 23:11; Kum 5:29; 6:5-6, 17

kumtumikia kwa moyo wenu wote na roho
yenu yote.”
6 [a]Ndipo Yoshua akawabariki na kuwaaga
waende zao, nao wakaenda nyumbani
mwao. 7 [b](Kwa nusu ya kabila la Manase
Mose alikuwa amewapa eneo katika
Bashani na ile nusu nyingine ya hilo
kabila Yoshua aliwapa eneo upande wa
magharibi ya Yordani pamoja na ndugu
zao). Yoshua alipowaaga waende zao
nyumbani, aliwabariki, 8 [c]akisema, “Rudini
nyumbani mwenu na utajiri wenu mwingi,
yaani makundi makubwa ya mifugo, mkiwa
na fedha, dhahabu, shaba na chuma, pia
wingi wa nguo, nanyi mkagawane na ndugu
zenu hizo nyara zilizotoka kwa adui zenu.”
9 [d]Kwa hiyo Wareubeni, Wagadi na hiyo
nusu ya kabila la Manase wakawaacha
Waisraeli huko Shilo katika nchi ya Kanaani
ili kurudi Gileadi, nchi yao wenyewe
waliyoipata sawasawa na agizo la BWANA
kupitia Mose.
10 [e]Walipofika Gelilothi karibu na Yordani,
katika nchi ya Kanaani, Wareubeni, Wagadi
na nusu ya kabila la Manase wakajenga
madhabahu ya fahari kubwa huko kando ya
Yordani. 11 [f]Waisraeli wengine waliposikia
kwamba Wareubeni, Wagadi na ile nusu
ya kabila la Manase walikuwa wamejenga
madhabahu kwenye mpaka wa Kanaani
huko Gelilothi karibu na Yordani kwenye
upande wa Israeli, 12 [g]kusanyiko lote
la Israeli wakakusanyika huko Shilo ili
wakapigane vita dhidi yao.
13 [h]Kwa hiyo Waisraeli wengine
wakamtuma Finehasi mwana wa kuhani
Eleazari katika nchi ya Gileadi, kwa
Wareubeni, Wagadi na hiyo nusu ya kabila
la Manase. 14 [i]Wakatuma pamoja naye watu
kumi ambao ni viongozi, mmoja kwa kila
kabila la Israeli, kila mmoja aliyekuwa
kiongozi katika mgawanyiko wa jamaa
miongoni mwa koo za Israeli.
15 Walipofika Gileadi, kwa Wareubeni,
Wagadi na nusu ya kabila la Manase,
wakawaambia: 16 [j]“Kusanyiko lote la BWANA
lasema: ‘Je, mmewezaje kuacha kumwamini
Mungu wa Israeli jinsi hii? Mmewezaje
kumwacha BWANA na kujijengea
madhabahu dhidi yake na kumwasi? 17 [k]Je,
dhambi ya Peori haikutosha? Hata ingawa
kulikuja tauni juu ya kusanyiko la BWANA,
mpaka leo hii hatujatakasika kutokana na
dhambi hiyo! 18 [l]Je, sasa ndiyo mnamwacha
BWANA?
“ ‘Kama mkimwasi BWANA leo, kesho
atalikasirikia kusanyiko lote la Israeli.
19 [m]Kama nchi mnayomiliki imenajisika,
vukeni mje katika nchi ya BWANA, mahali
Maskani ya BWANA ilipo, nanyi mkajitwalie
sehemu miongoni mwetu, lakini msije
mkaasi dhidi ya BWANA wala dhidi yetu
sisi kwa kujijengea madhabahu, zaidi
ya madhabahu ya BWANA Mungu wetu.
20 [n]Wakati Akani mwana wa Zera alipokosa
uaminifu kwa vitu vilivyowekwa wakfu,
je, ghadhabu haikulipata kusanyiko lote la
Israeli? Hakuwa yeye peke yake aliyekufa
kwa ajili ya dhambi yake.’ ”
21 Ndipo Wareubeni, Wagadi na nusu ya
kabila la Manase walipowajibu viongozi wa
koo za Israeli, wakisema: 22 [o]“Yeye Mwenye
Nguvu, Mungu, BWANA! Yeye Mwenye
Nguvu, Mungu, BWANA! Yeye anajua!
Israeli na wajue! Kama huu umekuwa ni
uasi au kukosa utii kwa BWANA, msituache
hai siku hii ya leo. 23 [p]Kama tumejijengea

[a]**22:6** Mwa 24:60; Kut 39:43; Mwa 47:7; Yos 14:13; 2Sam 6:18; Lk 24:50
[b]**22:7** Hes 32:19, 33; Yos 12:5; 17:2; 14:13; Lk 24:50
[c]**22:8** Kum 20:14; Hes 31:22, 27; Mwa 49:27; 1Sam 30:16; 2Sam 1:1; Isa 9:3
[d]**22:9** Yos 18:1; Hes 32:26
[e]**22:10** Yos 18:17; Isa 19:19; 56:7
[f]**22:11** Law 17:8; Kum 13:12; Amu 20:12
[g]**22:12** Yos 18:1
[h]**22:13** Hes 25:7; 25:7; Yos 24:33; Kum 13:14; Kut 6:25
[i]**22:14** Hes 1:4
[j]**22:16** Kum 7:3; 1Sam 15:11; Kum 12:13-14
[k]**22:17** Hes 23:28; 25:1-9
[l]**22:18** Law 10:6; Hes 16:22; Mwa 18:23-25; Yos 7:11-12; 2Sam 1:17; 1Nya 21:1, 14
[m]**22:19** Kut 26:1; Law 17:8-9; Yos 18:1
[n]**22:20** Yos 7:1; Za 7:11; Law 10:6; Yos 7:5
[o]**22:22** Kum 10:17; Za 50:1; 1Sam 2:3; 16:7; 1Fal 8:39; 1Nya 28:9; Za 11:4; 40:9; 44:21; 139:4; Yer 17:10; Ay 10:7
[p]**22:23** Yer 41:5; Kum 12:11; 1Sam 20:16; Za 7:3, 5, 10, 13, 14

madhabahu yetu wenyewe ili kumwacha
BWANA na kutoa sadaka za kuteketezwa
na sadaka za nafaka, au kutoa sadaka za
amani juu yake, BWANA mwenyewe na
atupatilize leo.
24 “Sivyo! Tulifanya hivyo kwa
hofu kwamba siku zijazo wazao wenu
wanaweza wakawaambia wazao wetu,
‘Mna uhusiano gani na BWANA, Mungu
wa Israeli? 25 BWANA ameifanya Yordani
kuwa mpaka kati yetu na ninyi, ninyi
Wareubeni na Wagadi! Hamna fungu kwa
BWANA.’ Kwa hiyo wazao wenu wanaweza
wakawasababisha wazao wetu wakaacha
kumcha BWANA.
26 “Hii ndiyo sababu tulisema, ‘Tujiweke
tayari na tujenge madhabahu, lakini si kwa
ajili ya sadaka za kuteketezwa au dhabihu.’
27 [a]Badala yake, itakuwa ni ushahidi kati
yetu na ninyi na vizazi vijavyo, kwamba
tutamwabudu BWANA katika mahali
patakatifu pake pamoja na sadaka zetu
za kuteketezwa, dhabihu na sadaka za
amani. Ndipo katika siku zijazo, wazao
wenu hawataweza kuwaambia wazao wetu,
‘Ninyi hamna fungu katika BWANA.’
28 [b]“Nasi tulisema, ‘Ikiwa wakati wowote
watatuambia hilo, au kuwaambia uzao
wetu, tutawajibu hivi: Angalieni nakala
hii ya madhabahu ya BWANA, ambayo
baba zetu waliijenga, si kwa ajili ya sadaka
za kuteketezwa na dhabihu, bali kama
ushahidi kati yetu na ninyi.’
29 [c]“Hili jambo la kumwasi BWANA na
kumwacha siku hii ya leo kwa kujenga
madhabahu kwa ajili ya sadaka za
kuteketezwa, sadaka za nafaka na dhabihu,
zaidi ya madhabahu ya BWANA Mungu
wetu iliyo mbele ya maskani yake na liwe
mbali nasi.”
30 Wakati kuhani Finehasi na viongozi
wa kusanyiko na wakuu wa koo za Israeli,
waliposikia hayo waliyosema Wareubeni,
Wagadi na Manase, wakaridhika. 31 [d]Naye
Finehasi mwana wa kuhani Eleazari,
akawaambia Wareubeni, Wagadi na
Manase, “Leo tunajua kwamba BWANA
yuko pamoja nasi, kwa sababu hamkukosa
uaminifu kwa BWANA katika jambo hili.
Sasa mmewaokoa Waisraeli na mkono wa
BWANA.”
32 Ndipo Finehasi, mwana wa kuhani
Eleazari na viongozi wakarudi Kanaani
kutoka kwenye kukutana kwao na Wareubeni
na Wagadi huko Gileadi nao wakatoa
taarifa kwa Waisraeli. 33 [e]Walifurahi kusikia
taarifa hiyo, na wakamhimidi Mungu. Wala
hawakuzungumza tena habari za kupigana
vita dhidi yao ili kuharibu nchi ambayo
Wareubeni na Wagadi waliishi.
34 [f]Nao Wareubeni na Wagadi wakayaita
yale madhabahu Edi, yaani Shahidi: kwa
kuwa itakuwa shahidi kati yetu na ninyi
kwamba BWANA ndiye Mungu.

### *Yoshua Anawaaga Viongozi*

23 [g]Baada ya muda mrefu kupita,
naye BWANA akawa amewapa
Israeli pumziko mbele ya adui zao wote
waliowazunguka, Yoshua, wakati huo
akiwa mzee na umri ukiwa umeendelea
sana, 2 [h]akawaita Israeli wote, wazee wao,
viongozi, waamuzi na maafisa Yoshua
akawaambia: “Mimi ni mzee na umri
wangu umeendelea sana. 3 [i]Ninyi wenyewe
mmeona kila kitu BWANA Mungu wenu,
alichowatendea mataifa haya yote kwa
ajili yenu. Ilikuwa ni BWANA Mungu
wenu aliyewapigania. 4 [j]Kumbukeni jinsi
nilivyowagawia kama urithi kwa makabila
yenu yote nchi ya mataifa yaliyobaki,
yaani mataifa niliyowashinda, kati ya
Mto Yordani na Bahari kuu upande
wa magharibi. 5 [k]BWANA Mungu wenu

[a]**22:27** Mwa 21:30; Yos 24:27; Isa 19:20; Kum 12:6
[b]**22:28** Mwa 21:30
[c]**22:29** Yos 24:16; Kut 26:1; Kum 12:13-14
[d]**22:31** Law 26:11-12; 2Nya 15:2; Kut 25:8; 29:45; Zek 8:23; Ufu 21:3
[e]**22:33** Dan 2:19; Lk 2:28; 1Nya 29:20; 29:30; Neh 8:6
[f]**22:34** Mwa 21:30; Yos 24:27
[g]**23:1** Kum 12:9; Yos 21:44; 13:1
[h]**23:2** Yos 7:6; 24:1; 13:1; Kum 31:28; 1Nya 28:1
[i]**23:3** Kut 14:14; Kum 20:4
[j]**23:4** Yos 19:51; Hes 34:2-6; Za 78:55
[k]**23:5** Amu 2:21; Za 44:5; Yer 46:15; Kut 23:30; 33:2

mwenyewe atawaondoa watoke mbele
yenu. Atawafukuza mbele yenu, nanyi
mtamiliki nchi yao, kama vile Bwana
Mungu wenu alivyowaahidi.
6 [a]“Kuweni hodari sana, kuweni
waangalifu kutii yote yaliyoandikwa
katika kitabu cha Sheria ya Mose, pasipo
kugeuka upande wa kuume au kushoto.
7 [b]Msishirikiane na mataifa yaliyobakia
katikati yenu, wala msiombe kwa majina ya
miungu yao au kuapa kwayo. Msiitumikie
wala kuisujudia. 8 [c]Bali mtashikamana kwa
uthabiti na Bwana, Mungu wenu, kama
vile ambavyo mmefanya mpaka sasa.
9 [d]“Bwana amewafukuza mbele yenu
mataifa makubwa na yenye nguvu, mpaka
siku ya leo hakuna yeyote aliyeweza
kusimama mbele yenu. 10 [e]Mtu mmoja
miongoni mwenu anafukuza watu elfu, kwa
kuwa Bwana Mungu wenu anawapigania,
kama alivyoahidi. 11 [f]Kwa hiyo kuweni
waangalifu sana kumpenda Bwana Mungu
wenu.
12 [g]“Lakini ikiwa mtageuka na
kushikamana na mabaki ya mataifa haya
yaliyosalia katikati yenu na kama mtaoana
na kushirikiana nao, 13 [h]basi mwe na hakika
kuwa Bwana Mungu wenu hatawafukuza
tena mataifa hayo mbele yenu. Badala yake,
watakuwa tanzi na mitego kwenu, mijeledi
migongoni mwenu, na miiba machoni
mwenu, mpaka mwangamie kutoka nchi
hii nzuri, ambayo Bwana Mungu wenu
amewapa.
14 [i]“Sasa mimi ninakaribia kwenda katika
njia ya watu wote wa dunia. Mnajua kwa
mioyo yenu na roho zenu kwamba hakuna
ahadi zozote njema Bwana Mungu wenu
alizowaahidia, ambazo hazikutimia. Kila
ahadi imetimizwa, hakuna hata moja
ambayo haikutimia. 15 [j]Lakini kama vile
kila ahadi njema ya Bwana Mungu wenu
imekuwa kweli, vivyo hivyo Bwana ataleta
maovu yote kama alivyo onya, mpaka awe
amewaangamiza kutoka nchi hii nzuri
aliyowapa. 16 [k]Kama mkilivunja agano la
Bwana Mungu wenu, ambalo aliwaamuru
ninyi, mkaenda na kuitumikia miungu
mingine na kuisujudia, hasira ya Bwana
itawaka dhidi yenu, nanyi mtaangamia
kutoka nchi nzuri aliyowapa ninyi.”

### *Agano Lafanywa Upya Huko Shekemu*

24 [l]Ndipo Yoshua akaita pamoja makabila
yote ya Israeli huko Shekemu.
Akawaita wazee, viongozi, waamuzi na
maafisa wa Israeli, nao wakaja mbele za
Mungu.
2 [m]Yoshua akawaambia watu wote, “Hili
ndilo Bwana, Mungu wa Israeli, asemalo:
‘Hapo zamani baba zenu, pamoja na Tera
baba yake Abrahamu na Nahori, waliishi
ng’ambo ya Mto nao waliiabudu miungu
mingine. 3 [n]Lakini nilimwondoa baba yenu
Abrahamu kutoka nchi hiyo ng’ambo ya
Mto, nami nikamwongoza katika nchi
yote ya Kanaani, nikampa wazao wengi.
Nikampa Isaki, 4 [o]naye Isaki nikampa
Yakobo na Esau. Esau nikampa nchi ya
vilima ya Seiri, lakini Yakobo pamoja na
wanawe wakashuka Misri.
5 [p]“ ‘Kisha nikawatuma Mose na Aroni,
nami nikawapiga Wamisri kwa kile
nilichokitenda huko, tena nikawatoa

[a]**23:6** Kum 28:6; 17:20; Yos 1:7; Kum 5:32
[b]**23:7** Kut 23:13; Yer 5:7; 12:16; Kut 20:5
[c]**23:8** Kum 10:20
[d]**23:9** Kum 11:23; 7:24
[e]**23:10** Law 26:8; Amu 3:31; Kut 14:14; Kum 3:22
[f]**23:11** Kum 4:15; Yos 2:15
[g]**23:12** Mwa 34:9; Kut 34:16; Za 106:34-35
[h]**23:13** Kut 10:7; Hes 33:55; Kum 1:8; 2Fal 25:21
[i]**23:14** 1Fal 2:2; Za 119:140; 145:13; Yos 21:25
[j]**23:15** 1Fal 8:56; Yer 33:14; 1Fal 14:10; 2Fal 22:16; Isa 24:6; 34:5; 43:28; Yer 40:2; 11:8; 35:17; 39:16; Mal 4:6; Yos 24:20; Law 26:17; Kum 28:15; Yer 40:2
[k]**23:16** Kum 4:25-26
[l]**24:1** Mwa 49:2; 12:6; 1Sam 12:7; 1Fal 8:14; Yos 7:6; 23:2; Amu 9:1-3; Kut 18:25; 1Sam 10:10; Mdo 10:33
[m]**24:2** Mwa 23:2; 11:32; Kum 26:5; Isa 51:2
[n]**24:3** Mwa 12:1; 1:28; 12:2; 21:3; Mdo 7:2; Za 127:3
[o]**24:4** Mwa 25:26; 14:6; Hes 24:18; Mwa 46:5-6; Kum 2:5; Mdo 17:26
[p]**24:5** Kut 3:10; 12:51

ninyi huko. 6 [a]Nilipowatoa baba zenu
Misri, mlifika kwenye bahari, nao Wamisri
wakawafuatia baba zenu kwa magari na
wapanda farasi mpaka kwenye Bahari
ya Shamu. 7 [b]Lakini wakamlilia BWANA
wakitaka msaada, naye akaweka giza kati
yenu na Wamisri, akaileta bahari juu yao
ikawafunika. Ninyi mliona kwa macho yenu
wenyewe kile nilichowatendea Wamisri.
Kisha mliishi jangwani kwa muda mrefu.
8 [c]“ ‘Nikawaleta katika nchi ya Waamori
ambao waliishi mashariki mwa Yordani.
Wakapigana nanyi, lakini nikawatia
mikononi mwenu. Nikawaangamiza mbele
yenu nanyi mkaimiliki nchi yao. 9 [d]Wakati
Balaki mwana wa Sipori, mfalme wa Moabu,
alipojiandaa kupigana dhidi ya Israeli,
alimwita Balaamu mwana wa Beori apate
kuwalaani. 10 [e]Lakini sikumkubali Balaamu,
kwa hiyo aliwabariki tena na tena, nami
niliwaokoa toka mkononi mwake.
11 [f]“ ‘Ndipo mlipovuka Yordani mkafika
Yeriko. Raiya wa Yeriko wakapigana nanyi,
kama walivyofanya Waamori, Waperizi,
Wakanaani, Wahiti, Wagirgashi, Wahivi
na Wayebusi, lakini niliwatia mikononi
mwenu. 12 [g]Nikatuma manyigu mbele yenu,
ambao pia waliwafukuza mbele yenu, hao
wafalme wawili wa Waamori. Siyo upanga
au upinde wenu wenyewe vilivyowapatia
ushindi. 13 [h]Hivyo nikawapa ninyi nchi
ambayo hamkuitaabikia na miji ambayo
hamkuijenga na mnaishi ndani yake na
kula toka kwa mashamba ya mizabibu na
mizeituni msiyoipanda.’
14 [i]“Sasa basi mcheni BWANA na
kumtumikia kwa uaminifu wote. Itupeni
mbali miungu ambayo baba zenu waliiabudu
huko ng’ambo ya Mto Frati na huko Misri,
nanyi mtumikieni BWANA. 15 [j]Lakini
msipoona vyema kumtumikia BWANA,
chagueni hivi leo mtakayemtumikia,
kama ni miungu ile ambayo baba zenu
waliitumikia ng’ambo Frati, au miungu
ya Waamori, ambao mnakaa katika nchi
yao. Lakini mimi na nyumba yangu,
tutamtumikia BWANA.”
16 [k]Ndipo hao watu wakajibu, “Hili jambo
liwe mbali nasi la kumsahau BWANA na
kuitumikia miungu mingine! 17 [l]BWANA
Mungu wetu mwenyewe ndiye alitutoa sisi
na baba zetu akatupandisha kutoka Misri,
kutoka nchi ile ya utumwa, na kutenda
zile ishara kubwa mbele ya macho yetu.
Ndiye aliyetulinda katika safari yetu yote na
kutokana na mataifa yote ambayo tulipita
katikati yao. 18 [m]BWANA akayafukuza mbele
yetu mataifa yote pamoja na Waamori,
walioishi katika nchi hii. Hivyo sisi nasi
tutamtumikia BWANA kwa kuwa yeye ndiye
Mungu wetu.”
19 [n]Yoshua akawaambia watu, “Hamwezi
kumtumikia BWANA. Yeye ni Mungu
Mtakatifu, ni Mungu mwenye wivu.
Hatasamehe uasi wenu na dhambi zenu.
20 [o]Ikiwa mkimwacha BWANA na kuitumikia
miungu migeni, atageuka na kuwaleteeni

[a]**24:6** Kut 14:22; 14:9; 4:23; Mik 6:4; Neh 9:11; Za 78:13; Isa 63:12, 13
[b]**24:7** Kut 14:10, 20, 28; 19:4; Kum 1:46
[c]**24:8** Kut 23:23; Hes 21:31
[d]**24:9** Hes 22:2, 6; 23:7
[e]**24:10** Hes 23:10; Kum 23:5
[f]**24:11** Kut 14:29; Yos 6:1; 3:10; Mwa 15:18-21; Kut 23:23; Kum 7:1
[g]**24:12** Kut 23:28; Za 44:3-7; Kut 23:31; Za 135:11; Kum 7:20
[h]**24:13** Kut 6:8; Kum 6:10-11; Yos 11:13; Mit 13:22
[i]**24:14** 1Sam 12:14; Ay 23:15; Za 19:9; 119:120; Kum 10:12; 18:13; 1Sam 12:24; 2Kor 1:20; Mwa 31:19; Kut 12:12; 18:11; 20:3; Hes 25:2; Kum 11:28; Amu 10:16; 10:16; Rut 1:15; Isa 55; 7; Eze 23; 3
[j]**24:15** Amu 6:10; Rut 1:15-16; 2:12; Mwa 35:2; 1Fal 18:21; Dan 3:18
[k]**24:16** Yos 22:29
[l]**24:17** Amu 6:8; Kut 10:1
[m]**24:18** Kut 23:31; Kum 33:27; Mdo 7:45; Mwa 28:21
[n]**24:19** Law 11:44; 20:26; Kut 20:5; 34:7; 23:21; Rut 1:15; Mt 6:24; Lk 14:25-33; Law 19:2; 1Sam 6:20; Za 99:5, 9; Isa 5:16; Kut 23:21
[o]**24:20** 1Nya 28:9, 20; 2Nya 24:18; Mdo 7:42; 1Sam 12:25; Hos 13:11; Yos 23:15; Ezr 8:22; Isa 1:28; 63:10; Yer 17:13; Ebr 10:26-28

maafa na kuwaangamiza, baada ya kuwa
mwema kwenu.”
21 Lakini watu wakamwambia Yoshua,
“Sivyo! Sisi tutamtumikia BWANA.”
22 [a]Ndipo Yoshua akawaambia, “Ninyi
mmekuwa mashahidi juu yenu wenyewe
kuwa mmechagua kumtumikia BWANA.”
Nao wakajibu, “Ndiyo, tu mashahidi.”
23 [b]Yoshua akawaambia, “Sasa basi,
itupeni mbali hiyo miungu migeni iliyo
katikati yenu, nanyi mtoleeni BWANA,
Mungu wa Israeli, mioyo yenu.”
24 [c]Nao watu wakamwambia Yoshua,
“Tutamtumikia BWANA Mungu wetu na
kumtii yeye.”
25 [d]Siku ile Yoshua akafanya agano kwa
ajili ya watu na hapo Shekemu ndipo
alipowaandikia amri na sheria. 26 [e]Naye
Yoshua akayaandika mambo haya katika
Kitabu cha Sheria ya Mungu. Ndipo
akalitwaa jiwe kubwa, akalisimamisha
huko chini ya mwaloni, karibu na mahali
patakatifu pa BWANA.
27 [f]Yoshua akawaambia watu wote,
“Angalieni! Jiwe hili litakuwa shahidi
juu yetu. Limesikia maneno yote BWANA
aliyotuambia. Litakuwa shahidi juu yenu
kama mtakuwa waongo kwa Mungu wenu.”

*Kuzikwa Katika Nchi Ya Ahadi*

28 [g]Basi Yoshua akawatuma watu kila
mmoja aende katika urithi wake mwenyewe.
29 [h]Baada ya mambo haya, Yoshua mwana
wa Nuni, mtumishi wa BWANA akafa akiwa
na umri wa miaka mia moja na kumi. 30 [i]Nao
wakamzika katika nchi ya urithi wake,
huko Timnath-Sera[j] katika nchi ya vilima
ya Efraimu, kaskazini ya Mlima wa Gaashi.
31 [k]Israeli wakamtumikia BWANA siku
zote za maisha ya Yoshua, na za hao wazee
walioishi baada ya Yoshua kufa, ambao
waliona kila kitu BWANA alichowatendea
Israeli.
32 [l]Nayo ile mifupa ya Yosefu, ambayo
Waisraeli waliipandisha kutoka huko Misri,
wakaizika huko Shekemu kwenye eneo,
ambalo Yakobo alilinunua kwa wana wa
Hamori baba yake Shekemu, kwa vipande
mia vya fedha. Eneo hili likawa ni urithi
wa uzao wa Yosefu.
33 [m]Naye Eleazari mwana wa Aroni
akafariki akazikwa huko Gibea, mlima
aliokuwa amepewa mtoto wake Finehasi,
kwenye nchi ya vilima ya Efraimu.

[a]**24:22** Rut 2:10; Isa 8; 2; 43:10; 44:8; Yer 42:5; Mal 2:14; Za 119:30, 173; Kum 25:9
[b]**24:23** 1Fal 8:58; Za 119:36; 141:4; Yer 31:33
[c]**24:24** Kut 19:8; Yer 42:6
[d]**24:25** Kut 24:8; Yos 17:7; Kut 15:25
[e]**24:26** Kum 17:18; 28:61; 31:24; Mwa 28:18; Kum 27:2; Mwa 12:6; Amu 4:11
[f]**24:27** Mwa 28:18; 21:30; Yos 22:27; 7:11; Hes 11:20; Mit 30:9
[g]**24:28** Amu 21:23-24
[h]**24:29** Amu 1:1; Mwa 50:22
[i]**24:30** Yos 19:50; 2Sam 23:30; Amu 2:7

[j]30 Unajulikana pia kama Timnath-Heresi, ona Yos 19:50; Amu 2:9.
[k]**24:31** Yos 7:6
[l]**24:32** Ebr 11:22; Mwa 47:29-30; 33:19; Yn 4:6; Mdo 7:16; Mwa 50:25; Kut 13:19
[m]**24:33** Yos 22:13; 15:57; Kut 6:25; 1Sam 9:4; 1Fal 8:4; Kut 6:25; Amu 20:28

# WAAMUZI

*Israeli Wapigana Na Wakanaani Waliobaki*

1 [a]Baada ya kifo cha Yoshua, Waisraeli
wakamuuliza BWANA, "Ni nani
atakayetangulia kupanda mbele yetu kwa
ajili ya kupigana na Wakanaani?"
2 [b]BWANA akajibu, "Yuda ndiye
atakayetangulia; nimewapa hiyo nchi
mikononi mwao."
3 Ndipo watu wa Yuda wakawaambia
Wasimeoni ndugu zao, "Pandeni pamoja nasi
katika nchi tuliyopewa, ili tupate kupigana
na Wakanaani. Sisi pia tutakwenda pamoja
nanyi katika sehemu yenu mliyopewa." Basi
Wasimeoni wakaenda pamoja nao.
4 [c]Yuda aliposhambulia, BWANA akawatia
Wakanaani na Waperizi mikononi mwao,
nao wakawaua watu 10,000 huko Bezeki.
5 Huko ndiko walipomkuta huyo Adoni-
Bezeki, nao wakapigana naye na kuwafanya
Wakanaani na Waperizi wakimbie. 6 Adoni-
Bezeki pia alikimbia, nao wakamfuata na
kumkamata, wakamkata vidole vyake
gumba vya mikono na vya miguu.
7 [d]Ndipo Adoni-Bezeki akasema,
"Nimewatendea wafalme sabini kama
nilivyotendewa na kuwalisha makombo ya
chakula chini ya meza yangu. Sasa Mungu
amenilipa haya, kama yale niliyowatendea."
Wakamleta Yerusalemu, naye akafa huko.
8 [e]Watu wa Yuda wakashambulia pia
Yerusalemu na kuiteka. Wakaupiga mji kwa
upanga na kuuchoma kwa moto.
9 [f]Baada ya hayo, watu wa Yuda
wakateremka kupigana na Wakanaani
walioishi katika nchi ya vilima, yaani,
Negebu na nchi chini ya vilima vya
magharibi. 10 [g]Yuda wakakabiliana na
Wakanaani walioishi Hebroni (ambayo
hapo kwanza iliitwa Kiriath-Arba) na
kuwashinda Sheshai, Ahimani na Talmai.
11 [h]Kutoka huko wakasonga mbele
kukabiliana na watu walioishi Debiri
(ambao hapo kwanza uliitwa Kiriath-
Seferi.) 12 Kalebu akasema, "Nitamwoza
binti yangu Aksa kwa mtu atakayeweza
kupigana na kuteka Kiriath-Seferi." 13 Basi
Othnieli mwana wa Kenazi, ndugu mdogo
wa huyo Kalebu, akawashinda, kwa hiyo
Kalebu akamtoa binti yake Aksa akaolewa
naye.
14 Siku moja Aksa alipokuja kwa Othnieli,
alimsihi Othnieli amwombe baba yake,
Kalebu, shamba. Aksa aliposhuka kutoka
juu ya punda wake, Kalebu akamuuliza,
"Je, wataka nikufanyie nini?"
15 [i]Akamjibu, "Naomba unifanyie jambo
moja la hisani. Kwa kuwa umenipa ardhi
huko Negebu, nipe pia chemchemi za maji."
Ndipo Kalebu akampa chemchemi za juu
na za chini.
16 [jk]Wazao wa yule Mkeni, baba mkwe
wa Mose, wakapanda pamoja na watu wa
Yuda kutoka Mji wa Mitende,[l] wakaenda
kuishi miongoni mwa watu wa jangwa ya
Yuda huko Negebu karibu na mji wa Aradi.
17 [m]Basi watu wa Yuda wakaenda na
Wasimeoni ndugu zao kushambulia
Wakanaani waishio Sefathi, nao
wakauangamiza huo mji kabisa. Kwa hiyo
huo mji ukaitwa Horma[n] 18 [o]Watu wa Yuda
wakatwaa pia Gaza, Ashkeloni na Ekroni,
kila mji na vijiji vyake vinavyouzunguka.
19 [p]BWANA alikuwa pamoja na watu wa
Yuda. Wakaimiliki nchi ya vilima, lakini

[a]**1:1** Yos 24:29; Hes 2:3-9; Amu 20:18; 1Fal 20:14; Mwa 10:18; Amu 3:1-6; Hes 27:21
[b]**1:2** Mwa 49:10; Amu 3:25; 4:7, 14; 7:9
[c]**1:4** Mwa 13:7; Yos 3:10; 1Sam 11:8
[d]**1:7** Law 24:19; Yer 25:12; Yos 10:1
[e]**1:8** Amu 1:21; Yos 15:63; 2Sam 5:6
[f]**1:9** Hes 13:17; Mwa 12:9; Hes 21:1; Isa 30:6
[g]**1:10** Mwa 13:18; 35:27; Hes 13:22; Yos 15:14
[h]**1:11** Yos 10:38
[i]**1:15** Hes 13:6
[j]**1:16** Hes 10:29; Mwa 15:19
[k]**1:16** Kum 34:3; Amu 3:13; 2Nya 28:15; Hes 21:1; Yos 12:14
[l]16 Yaani Yeriko.
[m]**1:17** Hes 14:45
[n]17 Horma maana yake ni Maangamizi.
[o]**1:18** Yos 11:22; 13:3
[p]**1:19** Hes 14:43; 13:17; Yos 17:16

hawakuweza kuwafukuza watu waliokaa
katika hiyo tambarare, kwa sababu
walikuwa na magari ya chuma. 20 [a]Kama
vile Mose alivyoahidi, Kalebu alipewa
Hebroni, naye akawafukuza wana watatu
wa Anaki. 21 [b]Hata hivyo, Wabenyamini
walishindwa kuwafukuza Wayebusi,
waliokuwa wanaishi Yerusalemu; hivyo
hadi leo Wayebusi huishi humo pamoja
na Wabenyamini.

22 [c]Basi nyumba ya Yosefu wakashambulia
Betheli, naye BWANA alikuwa pamoja nao.
23 [d]Walipotuma watu kwenda kupeleleza
Betheli (ambao hapo kwanza uliitwa Luzu),
24 [e]wale wapelelezi wakaona mtu anatoka
mjini, nao wakamwambia, “Tuonyeshe jinsi
ya kuingia mjini nasi tutakutendea wema.”
25 [f]Hivyo akawaonyesha, nao wakaupiga
mji kwa upanga lakini wakamhifadhi hai
yule mtu na jamaa yake yote. 26 [g]Yule mtu
akaenda hadi nchi ya Wahiti, ambapo
aliujenga mji na kuuita Luzu, ambao ndio
jina lake hadi leo.

27 [h]Lakini Manase hawakuwafukuza
watu wa Beth-Shani na vijiji vyake, au
watu wa Taanaki na vijiji vyake, au
watu wa Dori na vijiji vyake, au watu
wa Ibleamu na vijiji vyake, au watu wa
Megido na vijiji vyake, lakini Wakanaani
waliazimu kuishi katika nchi ile. 28 [i]Israeli
walipopata nguvu, wakawatia Wakanaani
katika kazi ya kulazimishwa, lakini
kamwe hawakuwafukuza watoke kabisa.
29 [j]Wala Efraimu hawakuwafukuza
kabisa Wakanaani walioishi Gezeri, bali
Wakanaani waliendelea kuishi humo
miongoni mwao. 30 Vivyo hivyo Zabuloni
hawakuwafukuza Wakanaani walioishi
huko Kitroni, wala walioishi Nahaloli,
ambao walibaki miongoni mwao; bali
waliwatia katika kazi ya kulazimishwa.
31 [k]Wala Asheri hawakuwafukuza wale
walioishi huko Ako, Sidoni, Alabu, Akzibu,
Helba, Afeki wala Rehobu 32 na kwa sababu
ya jambo hili Waasheri wakaishi miongoni
mwa Wakanaani, wenyeji wa nchi. 33 [l]Wala
Naftali hawakuwafukuza wale walioishi
Beth-Shemeshi wala wale walioishi Beth-
Anathi; lakini Naftali nao pia wakaishi
miongoni mwa Wakanaani, wenyeji wa
nchi, nao wale walioishi Beth-Shemeshi
na Beth-Anathi wakawa watumishi wao
katika kazi ya kulazimishwa. 34 [m]Waamori
wakawazuilia Wadani kwenye nchi
ya vilima, kwa maana hawakuwaacha
washuke kuingia kwenye sehemu
tambarare. 35 [n]Waamori pia wakaendelea
kukaa katika Mlima Heresi, katika Aiyaloni
na Shaalbimu, lakini mkono wa nyumba
ya Yosefu ukawalemea, nao wakashindwa
hata wakalazimika kuingia katika kazi
ya kulazimishwa. 36 [o]Mpaka wa Waamori
ulikuwa kuanzia Genge la Akrabimu,
kuendelea hadi Sela na kuelekea juu.

### *Malaika Wa BWANA Huko Bokimu*

2 [p]Malaika wa BWANA akakwea kutoka
Gilgali hadi Bokimu, naye akasema,
“Niliwapandisha kutoka Misri na kuwaingiza
katika nchi niliyoapa kuwapa baba zenu.
Nikasema, ‘Kamwe sitalivunja Agano langu
nanyi. 2 [q]Nanyi msifanye agano na watu
wa nchi hii, bali mtazibomoa madhabahu
yao.’ Lakini ninyi hamkunitii mimi. Kwa
nini mmefanya jambo hili? 3 [r]Sasa basi
ninawaambia kuwa sitawafukuza watoke

---

[a]**1:20** Yos 10:36; 14:13
[b]**1:21** Yos 9:15; 15:63
[c]**1:22** Amu 10:9; Yos 7:2
[d]**1:23** Mwa 28:19
[e]**1:24** Mwa 47:29; Yos 2:12-14
[f]**1:25** Yos 6:25
[g]**1:26** Kum 7:1; Eze 6:3; Mwa 19:19
[h]**1:27** 1Fal 9:21; Yos 11:2; 17:11; 12:21
[i]**1:28** Yos 17:12-13
[j]**1:29** Yos 14:4; Amu 5:14; Yos 10:33; 16:10
[k]**1:31** Yos 17:7; Mwa 49:13; Yos 15:44; 12:18; Hes 13:21
[l]**1:33** Yos 15:10; 19:38
[m]**1:34** Hes 13:29; Amu 10:11; 1Sam 7:14; Mwa 30:6; Amu 18:1
[n]**1:35** Amu 8:13; Yos 19:43; 1Fal 4:9
[o]**1:36** Yos 15:3; 2Fal 14:7; Isa 16:1; 42:11; Za 104:34
[p]**2:1** Mwa 16:7; Kum 11:30; Kut 20:2; Amu 6:8; Law 26:42-44; Kum 7:9
[q]**2:2** Kut 23:32; 34:12; Kum 7:2; Kut 23:24; 34:13; Kum 7:5; 2Nya 14:3; Yer 7:28
[r]**2:3** Yos 23:13; Hes 33:55; Kut 10:7; Za 106:36

katikati yenu ila watakuwa miiba kwenu,
nao miungu yao itakuwa tanzi kwenu.”
4 [a]Malaika wa BWANA alipomaliza
kusema mambo haya kwa Waisraeli wote,
watu wakalia kwa sauti kuu. 5 Wakapaita
mahali pale Bokimu. Nao wakamtolea
BWANA sadaka.

*Kifo Cha Yoshua*

6 Baada ya Yoshua kuwapa watu ruhusa
waende zao, Waisraeli wakaenda kwenye
urithi wao wenyewe ili kumiliki nchi yao.
7 Watu wakamtumikia BWANA siku zote
za maisha ya Yoshua, na za hao wazee
walioishi baada ya Yoshua kufa, waliokuwa
wameona mambo makuu ambayo BWANA
alikuwa ametenda kwa ajili ya Israeli.
8 Yoshua mwana wa Nuni, mtumishi wa
BWANA, akafa akiwa na umri wa miaka
110. 9 [b]Wakamzika katika nchi ya urithi
wake, huko Timnath-Heresi[c] katika nchi
ya vilima ya Efraimu, kaskazini ya Mlima
Gaashi.
10 [d]Baada ya kizazi kile chote kukusanywa
pamoja na baba zao, kikainuka kizazi
kingine baada yao ambacho hakikumjua
BWANA, wala matendo yale aliyokuwa
ametenda kwa ajili ya Waisraeli. 11 [e]Kwa
hiyo Waisraeli wakatenda maovu machoni
pa BWANA na kuwatumikia Mabaali.
12 [f]Wakamwacha BWANA, Mungu wa baba
zao, aliyekuwa amewatoa katika nchi ya
Misri. Wakaifuata na kuiabudu miungu
mbalimbali ya mataifa yanayowazunguka.
Wakamkasirisha BWANA, 13 [g]kwa sababu
walimwacha na kutumikia Baali na
Maashtorethi. 14 [h]Hivyo hasira ya BWANA
ikawaka juu ya Israeli, naye akawatia
mikononi mwa wavamizi waliowateka
nyara. Akawauza katika mikono ya adui
zao pande zote, hivyo hawakuweza tena
kuwazuia adui zao. 15 [i]Popote Israeli
walipotoka kwenda kupigana, mkono
wa BWANA ulikuwa kinyume nao ili
kuwashinda, kama vile alivyokuwa
amewaapia. Nao wakawa katika taabu
kubwa.
16 [j]Ndipo BWANA akawainua waamuzi,
ambao waliwaokoa katika mikono ya
hao watu waliowashambulia. 17 [k]Lakini
hawakuwasikiliza hata waamuzi wao, bali
walifanya uasherati kwa kuifuata miungu
mingine na kuiabudu. Waligeuka mara na
kuiacha njia ambayo baba zao waliiendea,
yaani, njia ya kutii amri za BWANA. 18 [l]Kila
mara BWANA alipowainulia mwamuzi,
BWANA alikuwa pamoja na huyo mwamuzi,
naye aliwaokoa kutoka mikononi mwa
adui zao kwa kipindi chote alichoishi yule
mwamuzi. Kwa kuwa BWANA aliwahurumia
kwa sababu ya kilio chao cha huzuni kwa
ajili ya wale waliokuwa wakiwatesa na
kuwataabisha. 19 [m]Lakini kila mara mwamuzi
alipofariki, watu walirudia katika hali
mbaya ya uovu zaidi kuliko baba zao,
wakiifuata miungu mingine kuitumikia na
kuiabudu. Walikataa kuacha matendo yao
maovu na njia zao za ukaidi.
20 [n]Kwa hiyo BWANA akawakasirikia
sana Israeli na kusema, “Kwa kuwa taifa

[a]**2:4** Mwa 27:38; Hes 25:6; 2Fal 17:13
[b]**2:9** Yos 19:50
[c]9 Unajulikana pia kama Timnath-Sera, ona Yos 19:50; 24:30.
[d]**2:10** 1Nya 28:9; Kut 5:2; Gal 4:8
[e]**2:11** 1Fal 15:26; Amu 3:12; 4:1; 6:1; 3:7; 8:33; 1Fal 16:31; 22:53; 2Fal 10:18; 17:16
[f]**2:12** Kum 32:12; Za 106:36; Kum 31:16; Amu 10:6; Hes 11:33; Kum 4:25; Za 78:5, 8; 106:40
[g]**2:13** 1Sam 7:3; 1Fal 11:5, 33; 2Fal 23:13; Amu 3:7; 5:8; 6:25; 8:33; 10:6; 1Sam 31:10; Neh 9:26; Za 78:56; Yer 11:10
[h]**2:14** Kum 31:17; Neh 9:27; Za 106:41; 44; 10; 89:41; Eze 34:8; Kum 32:30; Amu 3:8; Kum 28:25
[i]**2:15** Rum 1:13; Ay 19:21; 5:5; 20:22; Za 32:4; Mwa 35:3; 2Sam 22:7; 2Nya 15:4; Za 18:6
[j]**2:16** Rum 1; 1; 1Sam 4:18; 7:6, 15; 2Sam 7:11; 1Nya 17:10; Mdo 13:20; 1Sam 11:3; Za 106:43
[k]**2:17** Kut 34:15; Hes 15:39; Za 4:2; Neh 9:26; Za 106:36; Kum 9:12
[l]**2:18** 1Sam 7:3; 2Fal 13:5; Isa 19:20; 43:3, 11; 45:15, 21; 49:20; 60:16; 63:8; Hes 10:9; Kum 32:36; Kut 2:23
[m]**2:19** Mwa 6:11; Kum 4:16; 32:17; Neh 9:2; Za 78:57; Yer 44:9; Amu 4:1; 8:33; Kut 32:9
[n]**2:20** Kum 31:17; Yos 23:16; 7:11; 1Fal 17:15

hili limevunja Agano lile nililofanya
na baba zao na hawakunisikiliza,
21 [a]mimi nami sitafukuza taifa lolote
ambalo Yoshua aliliacha alipofariki.
22 [b]Nitayatumia ili nipate kuwapima
Israeli na kuona kama wataishika njia ya
Bwana na kuenenda katika hiyo kama
njia baba zao walivyofanya." 23 [c]Bwana
alikuwa ameyaacha hayo mataifa yabaki;
hakuyaondoa mara moja kwa kuyatia
mikononi mwa Yoshua.

*Mataifa Yaliyobaki Katika Ile Nchi*

3 [d]Haya ndiyo mataifa Bwana aliyoyaacha
ili kuwajaribu Waisraeli wote ambao
hawakujua vita vyovyote vya Kanaani
2 (alifanya hivi ili tu kuwafundisha wazao
wa Waisraeli ambao hawakuwa wamejua
vita hapo awali): 3 [e]wafalme watano wa
Wafilisti, Wakanaani wote, Wasidoni,
Wahivi waishio katika milima ya Lebanoni
kuanzia Mlima wa Baal-Hermoni hadi
Lebo-Hamathi. 4 [f]Waliachwa ili kuwajaribu
Waisraeli kuona kama wangetii amri za
Bwana, alizokuwa amewapa baba zao kwa
mkono wa Mose.

5 [g]Waisraeli wakaishi miongoni mwa
Wakanaani, Wahiti, Waamori, Waperizi,
Wahivi na Wayebusi. 6 [h]Wakawaoa binti
zao, nao wakawatoa binti zao waolewe
na wana wa hayo mataifa, na kuitumikia
miungu yao.

*Othnieli*

7 [i]Waisraeli wakafanya maovu machoni
pa Bwana, wakamsahau Bwana Mungu
wao na kutumikia Mabaali na Maashera.
8 [j]Hasira ya Bwana ikawaka dhidi ya Israeli,
hivyo akawauza na kuwatia mikononi mwa
Kushan-Rishathaimu mfalme wa Aramu-
Naharaimu[k] ambaye Israeli walikuwa chini
yake wakimtumikia kwa muda wa miaka
minane. 9 [l]Waisraeli walipomlilia Bwana,
yeye akawainulia mwokozi, Othnieli mwana
wa Kenazi, ndugu mdogo wa Kalebu,
ambaye aliwaokoa. 10 [m]Roho wa Bwana
akaja juu yake, hivyo akawa mwamuzi wa
Israeli, akaenda vitani. Bwana akamtia
Kushan-Rishathaimu mfalme wa Aramu
mikononi mwa Othnieli, naye akamshinda.
11 [n]Hivyo nchi ikawa na amani kwa muda
wa miaka arobaini, mpaka Othnieli mwana
wa Kenazi alipofariki.

*Ehudi*

12 [o]Waisraeli wakafanya maovu mbele za
Bwana tena, kwa kuwa walifanya maovu
hayo Bwana akamtia nguvu Egloni mfalme
wa Moabu dhidi ya Israeli. 13 [p]Egloni
akawataka Waamoni na Waamaleki
waungane naye, akaja kuishambulia Israeli,
nao wakatwaa Mji wa Mitende[q] 14 [r]Waisraeli
wakawa chini ya Egloni mfalme wa Moabu
kwa muda wa miaka kumi na minane.

15 [s]Waisraeli wakamlilia tena Bwana,
naye akawapa mwokozi: Ehudi, mtu wa
shoto, mwana wa Gera, Mbenyamini.
Waisraeli wakatuma kwa Egloni mfalme wa
Moabu ushuru kwa mkono wa Ehudi. 16 Basi

---

[a]**2:21** Yos 23:5
[b]**2:22** Mwa 22:1; Kut 15:25
[c]**2:23** Amu 1:1
[d]**3:1** Kut 15:25
[e]**3:3** Yos 13:2; Mwa 10:14; 10:17; Kut 3:8; Kum 3:8; Hes 13:21
[f]**3:4** Kut 12:25
[g]**3:5** Za 106:36; Yos 3:10; 11:3; Ezr 9:1
[h]**3:6** Ezr 10:18; Neh 13:23; Mal 2:11; Kut 34:16; Kum 7:3-4, 16
[i]**3:7** Kum 4:9; 32:18; Amu 8:34; Za 78:11; 106:7; Yer 23:27; Amu 2:11-13; 1Fal 16:33; 2Nya 34:7; Isa 17:8
[j]**3:8** Amu 2:14; Za 44:12; Isa 50:1; 52:3; Mwa 24:10
[k]8 Yaani Mesopotamia ya Kaskazini-Magharibi.
[l]**3:9** Amu 6:6-7; 10:10; 1Sam 12:10; Za 106:44; 107:13; Kum 28:29; Neh 9:27
[m]**3:10** Hes 11:25; Amu 6:34; 11:29; 13:25; 14:6; 15:14; 1Sam 11:6; 16:13; 1Fal 18:46; 1Nya 12:18; 2Nya 24:20; Isa 11:2; Mwa 10:22
[n]**3:11** Yos 14:15; Amu 5:31; 8:28; Kut 16:35; 15:17
[o]**3:12** Amu 2:11; 1Sam 12:9
[p]**3:13** Mwa 19:38; Amu 10:11; Mwa 14:7; Amu 1:16
[q]13 Yaani Yeriko.
[r]**3:14** Yer 48:1
[s]**3:15** Amu 1:4; 20:16; 1Nya 12:2; 2Sam 8:2-6; 1Fal 4:21; 2Fal 17:3; Es 10:1; Za 68:29; 72:10; 89:22; Mhu 2:8; Isa 60:5; Hos 10:6; Za 107:13

Ehudi alikuwa ametengeneza upanga wenye
ukatao kuwili, urefu wake ni kama dhiraa
moja,[a] akaufunga upanga huo ndani ya nguo
yake kwenye paja lake la mkono wa kuume.
17 [b]Akamkabidhi ushuru Egloni mfalme wa
Moabu, ambaye alikuwa mtu mnene sana.
18 Baada ya Ehudi kumkabidhi ule ushuru,
wale watu waliokuwa wameubeba huo
ushuru aliwaruhusu waende zao. 19 Yeye
mwenyewe akafuatana nao hadi kwenye
sanamu ya kuchora kwenye mawe karibu
na Gilgali, ndipo yeye akarudi, akafika
kwa Egloni na kusema, "Ee Mfalme, ninao
ujumbe wa siri kwa ajili yako."

Mfalme akasema, "Nyamazeni
kimya!" Nao wale waliomhudumia wote
wakamwacha, wakatoka nje.

20 [c]Ndipo Ehudi akamsogelea alipokuwa
ameketi peke yake kwenye chumba cha
juu cha jumba lake la kifalme la majira
ya kiangazi, na kusema, "Ninao ujumbe
kutoka kwa Mungu kwa ajili yako." Mfalme
alipokuwa anainuka kutoka kwenye kiti
chake, 21 [d]Ehudi akaunyoosha mkono wake
wa kushoto na kuufuta ule upanga aliokuwa
ameufunga kwenye paja lake la kulia,
akamdunga Mfalme Egloni tumboni mwake.
22 Hata mpini nao ukazama tumboni pamoja
na upanga wenyewe, nao upanga ukatokea
mgongoni mwake. Ehudi hakuuchomoa huo
upanga, nayo mafuta yakashikamana juu
ya upanga. 23 Ehudi akatoka nje barazani;
akamfungia milango ya chumba cha juu na
kuifunga kwa funguo.

24 [e]Baada ya kuondoka, watumishi wakaja
na kukuta milango ya chumba cha juu
imefungwa kwa funguo. Wakasema, "Bila
shaka amejipumzisha kwenye chumba
cha ndani cha nyumba yake ya majira ya
kiangazi." 25 [f]Wakangoja hata wakawa na
fadhaa, basi wakati hakufungua milango ya
chumba, wakachukua funguo na kuifungua.
Tazama wakaona bwana wao amelala
sakafuni, amekufa.

26 Walipokuwa wangali wanangoja, Ehudi
akatoroka, akapita hapo kwenye sanamu ya
kuchora kwenye mawe na kukimbilia Seira.
27 [g]Alipofika huko, akapiga tarumbeta katika
nchi ya vilima ya Efraimu, nao Waisraeli
wakateremka pamoja naye kutoka vilimani,
yeye akiwa anawaongoza.

28 [h]Akawaagiza, "Nifuateni, kwa
kuwa BWANA amewatia Moabu, adui
zenu, mikononi mwenu." Kwa hiyo
wakateremka wakamfuata, wakavishika
vivuko vya Yordani kuelekea Moabu, wala
hawakuacha mtu yeyote kuvuka. 29 Wakati
huo wakawaua Wamoabu watu waume
wapatao 10,000 ambao wote walikuwa
wenye nguvu na mashujaa; hakuna mtu
yeyote aliyetoroka. 30 [i]Siku ile Moabu
wakashindwa na Israeli, nayo nchi ikawa
na amani kwa miaka themanini.

*Shamgari*

31 [j]Baada ya Ehudi akaja Shamgari
mwana wa Anathi, aliyewapiga Wafilisti
600 kwa fimbo iliyochongoka ya kuongozea
ng'ombe. Naye pia akawaokoa Waisraeli.

*Debora*

4 [k]Baada ya Ehudi kufa, Waisraeli
wakafanya tena maovu machoni
pa BWANA. 2 [l]Hivyo BWANA akawatia
mikononi mwa Yabini, mfalme wa Kanaani,
aliyetawala huko Hazori. Jemadari wa
jeshi lake alikuwa Sisera, aliyeishi huko
Haroshethi-Hagoyimu[m] 3 [n]Kwa kuwa Sisera
alikuwa na magari ya chuma yapatayo
900, naye alikuwa amewatesa Waisraeli
kwa ukatili kwa muda wa miaka ishirini,

[a]16 Dhiraa moja ni sawa na sentimita 45.
[b]**3:17** Ay 15:27; Za 73:4
[c]**3:20** Amo 3:15; Neh 8:5
[d]**3:21** 2Sam 2:16; 3:27; 20:10
[e]**3:24** 1Sam 24:3
[f]**3:25** 2Fal 2:17; 8:11
[g]**3:27** Law 25:9; Amu 6:34; 7:18; 2Sam 2:28; Isa 18:3; Yer 42:14
[h]**3:28** Mwa 19:37; Yos 2:24; Amu 1:2; Hes 13:29; Yos 2:9
[i]**3:30** Mwa 36:35
[j]**3:31** Amu 5:6; Yos 23:10; 13:2; Amu 10:11; 13:1; 1Sam 5:1; 31:1; 2Sam 8:1; Yer 25:30; 47:1
[k]**4:1** Amu 3:15; 2:11; 2:19
[l]**4:2** Kum 32:30; Yos 11:1; 1Sam 12:9; Za 83:9
[m]2 Haroshethi-Hagoyimu ina maana Haroshethi ya Mataifa.
[n]**4:3** Yos 17:16; Amu 10:12; Za 106:42; Amu 1:19

Waisraeli wakamlilia BWANA wakaomba
msaada.
4 [a]Debora, nabii mwanamke, mkewe
Lapidothi, ndiye alikuwa anaamua Israeli
wakati ule. 5 [b]Debora alikuwa akiketi chini
ya Mtende wa Debora uliokuwa kati ya
Rama na Betheli katika nchi ya vilima ya
Efraimu, nao Waisraeli wakaja kwake ili
awaamue. 6 [c]Akatuma wamwite Baraka
mwana wa Abinoamu kutoka Kedeshi huko
Naftali na kumwambia, “BWANA, Mungu
wa Israeli, anakuagiza: ‘Nenda, chukua
wanaume 10,000 toka Naftali na Zabuloni,
mwende Mlima Tabori. 7 [d]Nitamshawishi
Sisera, jemadari wa jeshi la Yabini, pamoja
na magari yake na jeshi lake, hadi Mto
Kishoni na kumtia mikononi mwako.’ ”
8 Baraka akamwambia, “Ukienda pamoja
nami nitakwenda, lakini usipokwenda
pamoja nami, sitakwenda.”
9 [e]Debora akamwambia, “Hakika
nitakwenda pamoja nawe, lakini njia
unayoiendea haitakupa heshima wewe,
kwa kuwa BWANA atamtia Sisera mikononi
mwa mwanamke.” Hivyo Debora akaenda
pamoja na Baraka mpaka Kedeshi, 10 [f]mahali
ambapo Baraka aliwaita Zabuloni na
Naftali. Watu 10,000 wakamfuata Baraka,
na Debora pia akaenda pamoja naye.
11 [g]Basi Heberi, Mkeni, alikuwa
amejitenga na Wakeni wengine, yaani,
wazao wa Hobabu, mkwewe Mose, naye
akapiga hema lake karibu na ule mti
mkubwa wa mwaloni ulioko Saananimu,
karibu na Kedeshi.
12 [h]Sisera alipoambiwa kuwa Baraka
mwana wa Abinoamu alikuwa amepanda
Mlima Tabori, 13 [i]Sisera akakusanya pamoja
magari yake yote 600 ya chuma na watu
wote waliokuwa pamoja naye, kuanzia
Haroshethi-Hagoyimu mpaka Mto wa
Kishoni.
14 [j]Ndipo Debora akamwambia Baraka,
“Nenda! Hii ndiyo siku ambayo BWANA
amemtia Sisera mikononi mwako. Je,
BWANA hakukutangulia mbele yako?” Hivyo
Baraka akashuka kutoka Mlima Tabori,
akifuatwa na watu 10,000. 15 [k]BWANA
akamfadhaisha Sisera na magari yake yote,
pamoja na jeshi lake lote kwa upanga mbele
ya Baraka, naye Sisera akaliacha gari lake
na kukimbia kwa miguu. 16 [l]Lakini Baraka
akafuata magari pamoja na jeshi mpaka
Haroshethi-Hagoyimu. Jeshi lote la Sisera
likaanguka kwa upanga, wala hakuna hata
mtu mmoja aliyesalia.
17 [m]Sisera, hata hivyo, akakimbia kwa
miguu mpaka kwenye hema la Yaeli, mkewe
Heberi, Mkeni, kwa sababu palikuwa na
uhusiano wa kirafiki kati ya Yabini mfalme
wa Hazori na ukoo wa Heberi, Mkeni.
18 Yaeli akaenda kumlaki Sisera na
kumwambia, “Karibu, bwana wangu,
karibu ingia ndani kabisa. Usiogope.” Basi
Sisera akaingia ndani ya hema ya Yaeli,
naye akamfunika kwa blanketi nene.
19 [n]Akamwambia, “Nina kiu, tafadhali
nipe maji ya kunywa.” Ndipo akafungua
kiriba cha maziwa na kumpa akanywa,
kisha akamfunika.
20 Naye Sisera akamwambia, “Simama
mlangoni pa hema na mtu yeyote akija na
kukuuliza, ‘Je, kuna mtu yeyote hapa?’
sema, ‘Hapana.’ ”
21 [o]Ndipo Yaeli, mkewe Heberi, akatwaa
kigingi cha hema, akachukua nyundo
mkononi mwake, akamwendea polepole,

[a]**4:4** Amu 5:1, 7, 12; Kut 15:20
[b]**4:5** 1Sam 14:2; 22; 6; Yos 18:25; 12:5-9; Mwa 35:8
[c]**4:6** Amu 5:12-15; 1Sam 12:11; Ebr 11:32; Yos 12:22; Mwa 30:8; Amu 5:18; 6:35; Yos 19:22
[d]**4:7** Yos 11:1; Amu 5:12; 1Fal 18:40; Za 83:9; Amu 1:2
[e]**4:9** Yos 12:22; Amu 2:14
[f]**4:10** 2Nya 36:23; Ezr 1:2; Isa 41:2; 42:6; 45:3; 46:11; 48:15
[g]**4:11** Mwa 15:19; Hes 10:29; Yos 24:26; Amu 9:6; Yos 19:33
[h]**4:12** Yos 19:22
[i]**4:13** Yos 17:16; Amu 4:7; 5:19
[j]**4:14** Amu 1:2; Kum 9:3; 1Sam 8:20; 2Sam 5:24; Za 68:7
[k]**4:15** Kut 14:24; Za 18:14; Kut 14:28; Za 83:9-10
[l]**4:16** Kut 14:28; Za 83:9-10
[m]**4:17** Amu 5:6, 24; Mwa 15:19; Yos 11; 1
[n]**4:19** Mwa 18:8; Amu 5:25
[o]**4:21** Mwa 2:21; 15:12; 1Sam 26:12; Isa 29:10; Yon 1:5; Amu 5:26

akiwa amelala usingizi, akiwa amechoka.
Akakigongomea kile kigingi kwenye paji la
uso wake, kikapenya hata kuingia ardhini,
naye akafa.
22 [a]Baraka akakaribia akimfuatia Sisera,
Yaeli akatoka kumlaki. Akamwambia,
“Njoo, nitakuonyesha mtu unayemtafuta.”
Hivyo wakaingia ndani ya hema wakiwa
wamefuatana na tazama Sisera alikuwa
amelala humo, akiwa amekufa, na hicho
kigingi cha hema kikiwa kimegongomewa
kupitia paji la uso wake.
23 [b]Basi siku ile Mungu akamshinda
Yabini, mfalme wa Kanaani, mbele ya
Israeli. 24 [c]Nao mkono wa Waisraeli
ukaendelea kuwa na nguvu zaidi na zaidi
dhidi ya Yabini, mfalme wa Kanaani, mpaka
wakamwangamiza.

*Wimbo Wa Debora*

5 [d]Ndipo Debora na Baraka mwana wa Abinoamu wakaimba wimbo huu:

2 [e]“Wakuu katika Israeli
wanapoongoza,
wakati watu wanapojitoa
kwa hiari yao wenyewe:
mhimidini BWANA!

3 [f]“Sikieni hili, enyi wafalme!
Sikilizeni, enyi watawala!
Nitamwimbia BWANA, nitaimba;
kwa wimbo nitamhimidi BWANA,
Mungu wa Israeli.

4 [g]“Ee BWANA, ulipotoka katika Seiri,
ulipopita katika mashamba ya
Edomu,
nchi ilitetemeka, mbingu nazo
zikamwaga,
naam, mawingu yakamwaga maji.

5 [h]Milima ilitetemeka mbele za
BWANA,
hata ule wa Sinai,
mbele za BWANA,
Mungu wa Israeli.

6 [i]“Katika siku za Shamgari mwana wa
Anathi,
katika siku za Yaeli,
barabara kuu hazikuwa na watu;
wasafiri walipita njia za kando.
7 [j]Mashujaa walikoma katika Israeli,
walikoma mpaka mimi, Debora,
nilipoinuka,
nilipoinuka kama mama katika
Israeli.
8 [k]Walipochagua miungu migeni,
vita vilikuja katika malango ya
mji,
hapakuonekana ngao wala mkuki
miongoni mwa mashujaa 40,000
katika Israeli.
9 Moyo wangu u pamoja na wakuu wa
Israeli,
pamoja na wale wanaojitoa
wenyewe
kwa hiari yao miongoni mwa
watu.
Mhimidini BWANA!

10 [l]“Nanyi mpandao punda weupe,
mkiketi juu ya matandiko ya
thamani,
nanyi mtembeao barabarani,
fikirini 11 [m]juu ya sauti za waimbaji
mahali pa kunyweshea maji.
Wanasimulia matendo ya haki ya
BWANA,
matendo ya haki ya mashujaa
wake
katika Israeli.

“Ndipo watu wa BWANA
walipoteremka malangoni pa mji.

---

[a]**4:22** Amu 5:27
[b]**4:23** Neh 9:24; Za 18:47; 44:2; 47:3; 144:2; Yos 11; 1
[c]**4:24** Za 83:9; 106:43
[d]**5:1** Amu 4:4, 6; Kut 15:1; Za 32:7
[e]**5:2** 2Nya 17:16; Za 110:3
[f]**5:3** Kut 15:1; Za 27; 6
[g]**5:4** Kut 13:21; Hes 24:18; Kut 33:2; 2Sam 22:8; Za 18:7; 77:18; 82:5; Isa 2:19-21; 64:3; Yer 10; 10; 50:46; 51:29; Yoe 3:16; Nah 1:5; Hab 3:6; Za 68:8; 77:17
[h]**5:5** Kut 19:18; Za 29:6; 46:3; 77:18; 114:4; Isa 64:3
[i]**5:6** Amu 3:31; 4:17; Law 26:22; Isa 33:8; Za 125:5; Isa 59:8
[j]**5:7** Amu 4:4
[k]**5:8** Kum 32:17; Amu 2:13; Yos 2:5; Hes 25:7
[l]**5:10** Mwa 49:11; Amu 12:14; 10:4
[m]**5:11** 1Sam 12:7; Dan 9:16; Mik 6:5

12 [a]'Amka, amka! Debora!
Amka, amka, uimbe!
Ee Baraka! Inuka,
chukua mateka wako uliowateka,
ee mwana wa Abinoamu.'

13 "Ndipo mabaki ya watu
wakashuka dhidi ya wenye nguvu,
watu wa BWANA,
wakashuka dhidi ya mashujaa
wenye nguvu.
14 [b]Kutoka Efraimu wakaja watu,
ambao chimbuko lao ni
Amaleki;
Benyamini akiwa miongoni
mwa watu waliokufuata.
Kutoka Makiri wakashuka viongozi,
na kutoka Zabuloni wale washikao
fimbo ya jemadari.
15 [c]Wakuu wa Isakari walikuwa pamoja
na Debora;
naam, Isakari alikuwa pamoja na
Baraka,
wakija nyuma yake kwa mbio
wakielekea bondeni.
Katika jamaa za Reubeni,
palikuwa na kujihoji kukubwa
moyoni.
16 [d]Kwa nini ulikaa katikati ya mazizi
ya kondoo
kusikiliza sauti ya filimbi zinazoita
makundi?
Kwa jamaa za Reubeni,
palikuwa na kujihoji kukubwa
moyoni.
17 [e]Gileadi alikaa ng'ambo ya Yordani.
Naye Dani, kwa nini alikaa
kwenye merikebu siku nyingi?
Asheri alikaa kwa utulivu ufuoni
mwa bahari,
akikaa kwenye ghuba zake ndogo.
18 [f]Watu wa Zabuloni walihatarisha
maisha yao,
vilevile nao watu wa Naftali.

19 [g]"Wafalme walikuja na kufanya vita;
wafalme wa Kanaani walipigana
huko Taanaki karibu na maji ya
Megido,
lakini hawakuchukua fedha wala
nyara.
20 [h]Kutoka mbinguni nyota zilipigana,
nyota kutoka njia zake
zilipigana na Sisera.
21 [i]Mto wa Kishoni uliwasomba,
ule mto wa zamani, mto wa
Kishoni.
Songa mbele, ee nafsi yangu,
kwa ujasiri!
22 [j]Ndipo kwato za farasi zikafanya
mshindo:
farasi wake wenye nguvu
huenda mbio kwa kurukaruka.
23 Malaika wa BWANA akasema,
'Merozi alaaniwe.
Walaaniwe watu wake kwa
uchungu,
kwa kuwa hawakuja kumsaidia
BWANA,
kumsaidia BWANA dhidi ya hao
wenye nguvu.'

24 [k]"Yaeli abarikiwe kuliko wanawake
wote,
mkewe Heberi, Mkeni,
abarikiwe kuliko wanawake wote
waishio kwenye mahema.
25 [l]Aliomba maji, naye akampa
maziwa;
kwenye bakuli la heshima
akamletea maziwa mgando.
26 Akanyoosha mkono wake
akashika kigingi cha hema,

[a]**5:12** Za 44:23; 57:8; Isa 51:9, 17; Amu 4:4-6; Za 68:18; Efe 4:8
[b]**5:14** Mwa 41:52; Amu 1:29; 3:13; Hes 34:21; Mwa 50:23
[c]**5:15** Mwa 50:18; Amu 4:4-6
[d]**5:16** Mwa 49:11; Hes 32; 1
[e]**5:17** Yos 12:2; 17:7; 19:29
[f]**5:18** Mwa 30:20; 30:8; Za 68:27; Amu 9:6
[g]**5:19** Yos 11:5; Amu 4; 13; Ufu 16:16; Yos 12:21; Amu 1:27
[h]**5:20** Yos 10:11
[i]**5:21** Amu 4:7; Yos 1:6
[j]**5:22** Yer 8:16
[k]**5:24** Lk 1:42; Amu 4:17; Mwa 15:19
[l]**5:25** Mwa 18:8; Amu 4:19

mkono wake wa kuume
ukashika nyundo ya fundi.
Akampiga Sisera kwa nyundo,
akamponda kichwa chake,
akamvunjavunja na kumtoboa
paji lake la uso.
27 Aliinama miguuni pa Yaeli,
akaanguka; akalala hapo.
Pale alipoinama miguuni pake,
alianguka;
pale alipoinamia, ndipo alipoanguka,
akiwa amekufa.

28 [a]“Kupitia dirishani mamaye Sisera
alichungulia;
nyuma ya dirisha alilia, akasema,
‘Mbona gari lake linachelewa kufika?
Mbona vishindo vya magari yake
vimechelewa?’
29 Wanawake wenye busara
kuliko wengine wote wakamjibu;
naam, husema moyoni mwake,
30 [b]‘Je, hawapati na kugawanya nyara:
msichana mmoja au wawili kwa
kila mtu,
mavazi ya rangi mbalimbali kwa
Sisera kuwa nyara,
mavazi ya rangi mbalimbali
yaliyotariziwa,
mavazi yaliyotariziwa vizuri kwa
ajili ya shingo yangu:
yote haya yakiwa nyara?’

31 [c]“Adui zako wote na waangamie, Ee
Bwana!
Bali wote wakupendao na wawe
kama jua
lichomozavyo kwa nguvu zake.”

Hivyo nchi ikawa na amani kwa miaka arobaini.

*Gideoni*

6 [d]Waisraeli wakafanya tena yaliyo maovu
mbele za Bwana, naye kwa miaka
saba Bwana akawatia mikononi mwa
Wamidiani. 2 [e]Mkono wa Midiani ukawa
na nguvu dhidi ya Israeli na kwa ajili ya
Wamidiani, Waisraeli wakajitengenezea
mahali pa kujificha milimani, kwenye
mapango na ngome. 3 [f]Kila wakati
Waisraeli walipopanda mazao mashambani,
Wamidiani, Waamaleki na mataifa
mengine ya mashariki walivamia nchi yao.
4 [g]Wakapiga kambi katika mashamba yao na
kuharibu mazao ya nchi yote hadi kufikia
Gaza, wala hawakuacha kiumbe chochote
kilicho hai kwa Waisraeli, iwe kondoo au
ng’ombe au punda. 5 [h]Walipanda na mifugo
yao na mahema yao, mfano wa makundi
ya nzige. Ilikuwa haiwezekani kuwahesabu
watu na ngamia zao; wakavamia nchi ili
kuiharibu. 6 Waisraeli wakafanywa kuwa
maskini sana na Wamidiani, hata Israeli
wakamlilia Bwana kuomba msaada.
7 [i]Waisraeli walipomlilia Bwana
kwa sababu ya Wamidiani, 8 [j]Bwana
akawapelekea nabii, ambaye aliwaambia,
“Hili ndilo Bwana, Mungu wa Israeli,
asemalo: Niliwapandisha mtoke Misri, toka
nchi ya utumwa. 9 [k]Nikawanyakua kutoka
mikononi mwa Wamisri na kutoka mikononi
mwa watesi wenu wote. Nikawafukuza
watoke mbele yenu nami nikawapa ninyi
nchi yao. 10 [l]Nikawaambia, ‘Mimi ndimi
Bwana Mungu wenu; msiiabudu miungu
ya Waamori, ambayo mnakaa katika nchi
yao!’ Lakini ninyi hamkuitii sauti yangu.”

[a]**5:28** Yos 2:15; Mit 7:6
[b]**5:30** Kut 15:9; 1Sam 30:24; Za 68:12; 45:14; Eze 16:10; 2Sam 1:24
[c]**5:31** Hes 10:35; 2Sam 23:4; Ay 37:21; Za 19:4; 89:36; Isa 18:4; 2Sam 18:32; Amu 3:11
[d]**6:1** Amu 2:11; Mwa 25:2; Hes 25:15-18
[e]**6:2** 1Sam 13:6; Isa 5:30; 8:21; 26:16; 27:3; 2:19; Yer 48:28; 49:8; Ay 24:8; Yer 41:9; Ebr 11:38
[f]**6:3** Hes 13:29; Mwa 25:6; Isa 11:14; Yer 49:28
[g]**6:4** Law 26:16; Kum 28:30, 51; Isa 10:6; 42:22; Mwa 10:19
[h]**6:5** Kum 28:42; Amu 8:10; Isa 21:7; 60:6; Yer 49:28
[i]**6:7** Amu 3:9
[j]**6:8** Kum 18:15; 1Fal 20:13, 22; 2Fal 17:13, 23; Neh 9:29; Yer 25:5; Ay 36:10; Eze 18:30-31; Amu 2; 1
[k]**6:9** Neh 10:9; Za 136:24; 44:2
[l]**6:10** Kut 20:5; Yos 24:15; Yer 10:2

11 [a]Malaika wa BWANA akaja akaketi
chini ya mti wa mwaloni huko Ofra, ambao
ulikuwa mali ya Yoashi, Mwabiezeri, ambako
Gideoni mwanawe alikuwa akipepeta ngano
penye shinikizo la kukamulia zabibu, ili
kuificha Wamidiani wasiione. 12 [b]Malaika
wa BWANA alipomtokea Gideoni,
akamwambia, “BWANA yu pamoja nawe,
Ewe shujaa mwenye nguvu.”
13 [c]Gideoni akajibu, “Ee Bwana wangu,
kama BWANA yu pamoja nasi, mbona
mambo haya yote yametutokea? Yako
wapi basi yale matendo yake makuu baba
zetu waliyotusimulia juu yake waliposema,
‘Je, BWANA hakutupandisha kutoka Misri?’
Lakini sasa BWANA ametuacha na kututia
katika mkono wa Midiani.”
14 [d]BWANA akamgeukia na kusema
“Enenda kwa uwezo wako huu, ukawaokoe
Israeli kutoka mikononi mwa Wamidiani.
Je, si mimi ninayekutuma wewe?”
15 [e]Gideoni akauliza, “Ee Bwana wangu,
nitawezaje kuwaokoa Israeli? Ukoo wangu
ndio dhaifu kuliko zote katika Manase,
nami ndiye mdogo wa wote katika jamaa
yangu.”
16 [f]BWANA akamjibu, “Nitakuwa pamoja
nawe, nawe utawapiga Wamidiani kana
kwamba walikuwa ni mtu mmoja.”
17 [g]Gideoni akajibu, “Kama basi nimepata
kibali machoni pako, nipe ishara kuonyesha
kweli kwamba ni wewe unayesema nami.
18 Tafadhali ninakuomba usiondoke hapa
mpaka nitakaporudi na kukuletea sadaka
yangu na kuiweka mbele yako.”
Naye BWANA akamwambia, “Nitangoja
mpaka utakaporudi.”
19 [h]Gideoni akaingia ndani ya nyumba
yake na kuandaa mwana-mbuzi pamoja na
kuoka mikate isiyotiwa chachu kutokana
na efa moja[i] ya unga. Akaweka nyama
kwenye kikapu na mchuzi kwenye chungu,
akamletea huyo malaika hapo nje chini ya
mti wa mwaloni na kumpa.
20 [j]Malaika wa Mungu akamwambia,
“Itwae nyama na mikate isiyotiwa
chachu, uviweke juu ya mwamba huu na
umimine huo mchuzi juu yake.” Gideoni
akafanya hivyo. 21 [k]Malaika wa BWANA
akainyoosha fimbo iliyokuwa mkononi
mwake, ncha yake ikagusa ile nyama na
ile mikate isiyotiwa chachu, nao moto
ukatoka kwenye mwamba ukateketeza
ile nyama na ile mikate. Malaika wa
BWANA akatoweka kutoka machoni pake.
22 [l]Gideoni alipotambua kuwa ni malaika
wa BWANA, akapiga kelele kwa mshangao,
akasema, “Ole wangu, BWANA Mwenyezi!
Kwa kuwa nimemwona malaika wa BWANA
uso kwa uso!”
23 [m]Lakini BWANA akamwambia, “Amani
iwe kwako! Usiogope. Hutakufa.”
24 [n]Hivyo Gideoni akamjengea BWANA
madhabahu mahali pale na kupaita, Yehova-
Shalom.[o] Mpaka leo ingalipo imesimama
huko Ofra ya Waabiezeri.
25 [p]Usiku ule ule BWANA akamwambia,
“Mchukue ng’ombe dume wa baba yako,
yaani, yule wa pili mwenye miaka saba,
na ubomoe madhabahu ya Baali aliyo nayo
baba yako, na ukaikate Ashera iliyo karibu
nayo. 26 [q]Kisha mjengee BWANA Mungu
wako, madhabahu halisi, kwa taratibu zake,
juu ya huu mwamba. Kwa kutumia kuni za
hiyo nguzo ya Ashera uliyoikatakata, mtoe
sadaka huyo dume wa pili kuwa sadaka ya
kuteketezwa.”
27 Basi Gideoni akawachukua watumishi

[a]**6:11** Mwa 16:7; Yos 18:23; Amu 7:14; 8:13, 29; Hes 26:30; Amu 7:1; 8; 1; Ebr 11:32; Rut 2:17; 3:2; 1Sam 23:1; Neh 13:15; Isa 16:10; 63:3; Mao 1:15; Yoe 3:13
[b]**6:12** Yos 1:5; Rut 2:4; 1Sam 10:7; Za 129:8; Amu 11:1; Lk 1:11, 28
[c]**6:13** Yos 3:5; 2Sam 7:22; Za 44; 1; 78:3; Kum 31:17; 2Nya 15; 2
[d]**6:14** Ebr 11:34; Amu 10:1; 1Fal 14:27
[e]**6:15** Isa 60:22; 1Sam 9:20-21
[f]**6:16** Kut 3:12; Hes 14:43; Yos 1:5
[g]**6:17** Mwa 24:14; Kut 3; 12; 4:8
[h]**6:19** Mwa 18:7-8; Law 19:36; Amu 13:15
[i]19 Efa moja ni sawa na lita 22.
[j]**6:20** Amu 13:19
[k]**6:21** Kut 4:2; Law 9:24
[l]**6:22** Kum 13:16; Mwa 32:30; 11:32
[m]**6:23** Dan 10:19; Mwa 16:13; Kum 5:26
[n]**6:24** Mwa 22:14; Yos 18:23
[o]24 Yehova-Shalom maana yake Bwana ni Amani.
[p]**6:25** Kut 34:13; Amu 2:13; Kum 2:13; 7:5
[q]**6:26** Mwa 8:20

wake kumi na kufanya kama Bwana
alivyomwambia. Lakini kwa kuwa
aliwaogopa jamaa yake na watu wa mji,
akafanya haya usiku badala ya mchana.
28 [a]Watu wa mji walipoamka asubuhi,
tazama madhabahu ya Baali imebomolewa
na nguzo ya Ashera iliyokuwa karibu nayo
imekatwakatwa na yule ng'ombe wa pili
ametolewa sadaka juu ya madhabahu
yaliyojengwa upya!
29 Wakaulizana, "Ni nani aliyetenda
mambo haya?"
Walipochunguza kwa makini,
wakaambiwa, "Ni Gideoni mwana wa
Yoashi, ndiye alitenda hivi."
30 Watu wa mji wakamwambia Yoashi,
"Mlete mwanao hapa. Ni lazima afe, kwa
sababu amebomoa madhabahu ya Baali
na kukatakata nguzo ya Ashera iliyokuwa
karibu nayo."
31 [b]Lakini Yoashi akauambia ule umati
uliokuwa umezunguka ukiwa kinyume
naye, "Je, ninyi mtamtetea Baali? Mnajaribu
kumwokoa? Yeyote mwenye kumpigania
atauawa kufikia kesho asubuhi! Kama
Baali ni mungu kweli, anaweza kujitetea
mwenyewe wakati mtu anapobomoa
madhabahu yake."
32 [c]Basi siku ile
wakamwita Gideoni "Yerub-Baali," yaani,
"Baali na ashindane naye," kwa sababu
alibomoa madhabahu yake.
33 [d]Basi Wamidiani wote, Waamaleki
na mataifa mengine ya mashariki
wakaunganisha majeshi yao, wakavuka
ng'ambo ya Yordani na kupiga kambi
katika Bonde la Yezreeli.
34 [e]Ndipo Roho
wa Bwana akamjia Gideoni, akapiga
tarumbeta, akiwaita Waabiezeri ili
wamfuate.
35 [f]Akatuma wajumbe waende
katika Manase yote, akiwataka wachukue
silaha na pia katika Asheri, Zabuloni na
Naftali, nao wakakwea ili kukutana nao.
36 Gideoni akamwambia Mungu, "Kama
utawaokoa Waisraeli kwa mkono wangu,
kama ulivyoahidi:
37 [g]tazama, nitaweka
ngozi ya kondoo kwenye kiwanja cha
kupuria nafaka, na kama utakuwepo
umande juu ya ngozi tu, nayo ardhi yote
ikiwa kavu, ndipo nitakapojua kuwa
utaokoa Israeli kwa mkono wangu, kama
ulivyosema."
38 Hivyo ndivyo ilivyotokea.
Gideoni akaamka asubuhi na mapema
kesho yake, akaikamua ile ngozi, umande
ukatoka, maji ya kujaa bakuli.
39 [h]Kisha Gideoni akamwambia Bwana,
"Usinikasirikie. Ninaomba nifanye ombi
moja lingine. Niruhusu nifanye jaribio
jingine moja kwa ngozi hii. Wakati huu
uifanye ngozi hii kavu na ardhi yote
ifunikwe na umande."
40 [i]Usiku ule Mungu
akafanya hivyo. Ngozi ile ilikuwa kavu,
nayo ardhi yote ikafunikwa na umande.

*Gideoni Awashinda Wamidiani*

7 [j]Ndipo Yerub-Baali (yaani Gideoni)
na lile jeshi lililokuwa pamoja naye,
wakaondoka asubuhi na mapema na kupiga
kambi kando ya chemchemi ya Harodi.
Kambi ya Wamidiani ilikuwa kaskazini yao
katika bonde karibu na kilima cha More.
2 [k]Bwana akamwambia Gideoni, "Jeshi
lililo pamoja nawe ni kubwa sana kwa
mimi kuwatia Wamidiani mikononi mwao.
Ili kwamba Israeli asije akajisifu juu yangu
akisema, 'Mkono wangu ndio ulioniokoa,
3 [l]kwa hiyo sasa tangaza jeshi lote likiwa
linasikia, kwamba: Yeyote anayeogopa
na kutetemeka, yeye na arudi nyumbani,
aondoke katika Mlima Gileadi.' " Hivyo
watu 22,000 walirudi, wakabaki 10,000.
4 [m]Lakini Bwana akamwambia Gideoni,
"Idadi ya jeshi bado ni kubwa. Wapeleke
chini katika maji nami nitawajaribu huko

[a]**6:28** 1Fal 16:32; 2Fal 21:3
[b]**6:31** 1Sam 24:15; Za 43:1; Yer 30:13
[c]**6:32** Amu 7:1; 8:29, 35; 9:1; 1Sam 12:11
[d]**6:33** Hes 13:29; Mwa 25:6; Yos 15:56; Eze 25:4; Hos 1:5
[e]**6:34** Amu 3:10; Yos 6:20; Amu 3:27; Yos 17:2
[f]**6:35** Yos 17:7; Amu 4:6; 7:23
[g]**6:37** Ay 31:20; Hes 18; 27; 2Sam 6:6; 24:16; Mwa 24; 14
[h]**6:39** Mwa 18:32
[i]**6:40** Kut 4:3-7; Isa 28:7
[j]**7:1** Amu 6:32; 6:11; 2Sam 23:25; Mwa 25:2; 12:6
[k]**7:2** Kum 8:17; 2Kor 4:7
[l]**7:3** Kum 20:8; Yos 12:2
[m]**7:4** 1Sam 14:6

kwa ajili yako. Kama nikikuambia, ‘Huyu
atakwenda pamoja nawe,’ yeye atakwenda;
lakini kama nikisema, ‘Huyu hatakwenda
pamoja nawe,’ yeye hatakwenda.”
5 Hivyo Gideoni akalileta lile jeshi chini
kwenye maji naye BWANA akamwambia
Gideoni, “Watenge upande mmoja wale
wote wanywao maji kwa ulimi, kama
vile mbwa anywavyo, wale wote wapigao
magoti ili kunywa wakipeleka mikono
yao vinywani mwao, waweke upande
mwingine.” 6 [a]Idadi ya wale waliokunywa
kwa kuramba ramba walikuwa 300, lakini
wengine wote katika jeshi walipiga magoti
ili kunywa.
7 [b]BWANA akamwambia Gideoni, “Kwa
hao watu 300 walioramba maji nitawaokoa
ninyi, nami nitawatia Wamidiani mkononi
mwako. Waache hao watu wengine wote
warudi kila mmoja nyumbani mwake.”
8 Hivyo Gideoni akawaacha wale Waisraeli
wengine kila mmoja aende kwenye hema
yake. Akabakia na wale 300, ambao
walichukua vyakula na tarumbeta za wale
wenzao.
Basi kambi ya Wamidiani ilikuwa chini
yake bondeni. 9 [c]Usiku ule ule BWANA
akamwambia Gideoni, “Ondoka, ushuke
kambini, kwa kuwa nimeitia mkononi
mwako. 10 Lakini kama unaogopa
kushambulia, shuka kambini pamoja na
mtumishi wako Pura, 11 nawe sikiliza
wanayosema. Hatimaye, utatiwa moyo
kushambulia kambi.” Basi yeye na Pura
mtumishi wake wakashuka na kufikia
walinzi wa mbele wenye silaha waliokuwa
mle kambini. 12 [d]Wamidiani, Waamaleki na
mataifa mengine yote ya mashariki walikaa
bondeni, nao walikuwa mfano wa nzige kwa
wingi wao. Ngamia zao hazikuhesabika,
wingi wao ulikuwa kama mchanga wa
ufuoni mwa bahari.
13 Gideoni alifika wakati huo huo kukiwa
na mtu mmoja aliyekuwa anamweleza
mwenzake ndoto yake, akisema, “Niliota
ndoto: Tazama mkate wa shayiri
ulioviringana ulianguka katika kambi moja
ya Wamidiani, ukaipiga na ikaanguka nao
ukaipindua juu chini na hema ikaporomoka
chini.”
14 [e]Rafiki yake akamjibu, “Habari hii si
kitu kingine zaidi ya upanga wa Gideoni
mwana wa Yoashi, Mwisraeli. Mungu
amewatia Wamidiani na jeshi lote mkononi
mwake.”
15 [f]Gideoni alipoisikia hiyo ndoto
na tafsiri yake, akamwabudu Mungu.
Akarudi kwenye kambi ya Israeli na
kusema, “Inukeni! BWANA amelitia
jeshi la Wamidiani mikononi mwenu.”
16 [g]Akawagawa wale watu 300 katika
makundi matatu, akawakabidhi tarumbeta
mikononi mwao wote na mitungi isiyokuwa
na maji yenye mienge ndani yake.
17 Akawaambia, “Nitazameni, fanyeni
kama nitakavyofanya, nitakapofika mwisho
wa kambi mfanye kama nitakavyofanya.
18 [h]Wakati mimi na wale walio pamoja
nami wote, tutakapopiga tarumbeta zetu,
ninyi nanyi pigeni tarumbeta pande zote
za kambi na mpige kelele, mseme, ‘Upanga
wa BWANA na wa Gideoni.’ ”
19 Gideoni na wale watu 100 waliokuwa
pamoja naye wakafika mwisho wa kambi
usiku mwanzoni mwa zamu ya kati,
mara tu walipokuwa wamebadili zamu.
Wakapiga zile tarumbeta zao na kuvunja ile
mitungi iliyokuwa mikononi mwao. 20 [i]Yale
makundi matatu yakapiga tarumbeta na
kuvunja mitungi. Wakashika mienge kwa
mikono yao ya kushoto na katika mikono
yao ya kuume tarumbeta ili kuzipiga,
wakapaza sauti zao, “Upanga wa BWANA
na wa Gideoni!” 21 [j]Wakasimama kila mtu
mahali pake kuizunguka kambi pande
zote, Wamidiani wote wakakimbia, huku
wakipiga kelele.

---

[a]**7:6** Mwa 14:14
[b]**7:7** Yos 8:7; 1Sam 14:6
[c]**7:9** Yos 2:24; Amu 1:2
[d]**7:12** Hes 13:29; Kum 28:42; Yer 46:23; 49:29; Yos 11:4
[e]**7:14** Amu 6:11
[f]**7:15** 1Sam 15:31
[g]**7:16** Mwa 14:15; Amu 9:43; 1Sam 11:11; 2Sam 18:2; Law 25:9; Mwa 24:14; 15:17
[h]**7:18** Amu 3:27
[i]**7:20** Mwa 15:17; Kum 32:41
[j]**7:21** 2Fal 7:7

22 [a]Walipozipiga zile tarumbeta 300, Bwana akafanya watu katika kambi yote kugeuziana upanga kila mmoja na mwenziwe. Jeshi likakimbia mpaka Beth-Shita kuelekea Serera[b] hadi mpakani mwa Abel-Mehola karibu na Tabathi. 23 [c]Watu wa Israeli wakaitwa kutoka Naftali, Asheri na Manase, wakawafuatia Wamidiani. 24 [d]Gideoni akatuma wajumbe katika nchi yote ya vilima vya Efraimu akisema, "Teremkeni dhidi ya Wamidiani na mkazuie vivuko vya maji mbele yao hadi Beth-Bara na pia Yordani."

Hivyo watu wote wa Efraimu wakakutanika pamoja na kuzingira mto wa Yordani hadi Beth-Bara. 25 [e]Wakawakamata wakuu wawili wa Midiani, Orebu na Zeebu. Wakamuulia Orebu pale penye mwamba wa Orebu, na Zeebu wakamuulia penye shinikizo la kukamulia divai la Zeebu. Wakawafuatia Wamidiani na kuleta vichwa vya Orebu na Zeebu kwa Gideoni, huko ng'ambo ya Yordani.

*Ushindi Wa Gideoni Na Kulipiza Kisasi*

8 [f]Basi Waefraimu wakamuuliza Gideoni, "Mbona mmetutenda hivi? Kwa nini hukutuita ulipokwenda kupigana na Wamidiani?" Wakawalaumu kwa ukali sana.

2 [g]Gideoni akawajibu, "Nilichofanya mimi ni nini kulinganisha na kile ninyi mlichofanya? Je, kuokoa masazo ya zabibu za Efraimu si bora kuliko mavuno kamili ya zabibu ya Abiezeri? 3 [h]Mungu amewatia Orebu na Zeebu, hao viongozi wa Wamidiani, mikononi mwenu. Je, mimi niliweza kufanya nini kulinganisha na mlichofanya ninyi?" Aliposema hili, hasira yao dhidi yake ikatulia.

4 [i]Gideoni akiwa pamoja na wale watu 300 waliofuatana naye, wakiwa wamechoka na wenye njaa lakini bado wakiwafuatia, wakafika Yordani na kuuvuka. 5 [j]Akawaambia watu wa Sukothi, "Tafadhali lipatieni jeshi langu mikate, kwa maana wamechoka, nami ningali ninawafuatia Zeba na Salmuna, wafalme wa Midiani."

6 [k]Lakini maafisa wa Sukothi wakasema, "Je, mikono ya Zeba na Salmuna tayari mnayo sasa ili tuweze kulipatia jeshi lako mikate?"

7 Gideoni akajibu, "Kwa ajili ya hilo tu, Bwana atakapowatia Zeba na Salmuna mkononi mwangu, nitaichana nyama ya miili yenu kwenye miiba ya nyikani na kwenye michongoma."

8 [l]Kutoka hapo alikwea mpaka Penieli na kutoa ombi lile lile, lakini nao watu wa Penieli wakamjibu kama watu wa Sukothi walivyokuwa wamemjibu. 9 Hivyo akawaambia watu wa Penieli, "Nitakaporudi baada ya kushinda, nitaubomoa mnara huu."

10 [m]Wakati huu Zeba na Salmuna walikuwa Karkori wakiwa na jeshi lenye watu wapatao 15,000 wale wote waliokuwa wamesalia wa mataifa ya mashariki, kwa kuwa watu wapatao 120,000 wenye panga walikuwa wameuawa. 11 [n]Basi Gideoni akakwea kwa njia ya wasafiri mashariki ya Noba na Yogbeha na kulishambulia jeshi ambalo halikushuku lolote. 12 Zeba na Salmuna, hao wafalme wawili wa Midiani, wakakimbia lakini yeye Gideoni akawafuata na kuwakamata, akalishinda hilo jeshi lao lote.

13 [o]Gideoni mwana wa Yoashi akarudi kutoka vitani kwa kupitia Mwinuko wa

[a]**7:22** Yos 6:20; 1Sam 14:20; 2Nya 20:23; Isa 9:21; 19:2; Eze 38:21; Hag 2:22; Zek 14:13; Hab 3:14; 1Sam 18:19; 1Fal 4:12; 2Fal 19:16
[b]22 Au: Seretha.
[c]**7:23** Yos 17:7; Amu 6:35; Za 83:9
[d]**7:24** Yos 2:7
[e]**7:25** Amu 8:3; Za 83:11; Isa 10:26; 9:4; Amu 8:4; Za 106:43
[f]**8:1** Amu 6:11; Mwa 25:2; Amu 12:1; 2Sam 19:41
[g]**8:2** Hes 26:30
[h]**8:3** Amu 7:25; Mit 15:1
[i]**8:4** Amu 7:25
[j]**8:5** Mwa 33:17; Za 83:11; Yer 45:3; Ay 16:7; Za 6:6
[k]**8:6** 1Sam 25:11
[l]**8:8** Mwa 32:30; 1Fal 12:25
[m]**8:10** Amu 6:5; Isa 9:4
[n]**8:11** Hes 32:42; 32:35
[o]**8:13** Amu 6:11; 1:35

Heresi. [14] [a]Akamkamata kijana mmoja wa
Sukothi na kumuuliza maswali, naye yule
kijana akamwandikia majina ya maafisa
sabini wa Sukothi, ambao ni viongozi wa
mji. [15] Ndipo Gideoni akaja na kuwaambia
watu wa Sukothi, “Tazama, hapa wapo Zeba
na Salmuna mlionisimanga kwa ajili yao
mkisema, ‘Je, mikono ya Zeba na Salmuna
tayari mnayo sasa ili tuweze kulipatia
jeshi lako mikate?’ ” [16] [b]Akawachukua hao
viongozi wa mji na kuwafundisha watu
wa Sukothi somo kwa kuwaadhibu kwa
miiba na michongoma ya nyikani. [17] Pia
akaubomoa mnara wa Penieli na kuwaua
watu wa mji.

[18] [c]Kisha akawauliza Zeba na Salmuna,
“Ni watu wa aina gani mliowaua huko
Tabori?”

Wakajibu, “Ni watu kama wewe, kila
mmoja wao akiwa na nafasi ya uana wa
mfalme.”

[19] [d]Gideoni akajibu, “Hao walikuwa ndugu
zangu, wana wa mama yangu hasa. Hakika
kama aishivyo BWANA, kama mngekuwa
mmewaacha hai, mimi nisingewaua ninyi.”
[20] Akamgeukia Yetheri, mwanawe mzaliwa
wa kwanza, akasema, “Waue hawa!” Lakini
Yetheri hakuufuta upanga wake, kwa
sababu aliogopa, kwa kuwa alikuwa bado
kijana mdogo tu.

[21] [e]Zeba na Salmuna wakasema, “Njoo
ufanye hivyo wewe mwenyewe. ‘Alivyo
mtu, ndivyo zilivyo nguvu zake.’ ” Hivyo
Gideoni akatoka mbele na kuwaua, naye
akayaondoa mapambo kwenye shingo za
ngamia zao.

*Kisibau Cha Gideoni*

[22] Waisraeli wakamwambia Gideoni,
“Ututawale, wewe, wanao na wana wa
wana wako, kwa kuwa umetuokoa kutoka
mikononi mwa Wamidiani.”

[23] [f]Lakini Gideoni akawaambia, “Mimi
sitatawala juu yenu, wala wanangu
hawatatawala juu yenu. BWANA ndiye
atakayetawala juu yenu ninyi.” [24] [g]Naye
akasema, “Ninalo ombi moja, kwamba kila
mmoja wenu anipatie kipuli kutoka kwenye
fungu lake la nyara.” (Ilikuwa desturi ya
Waishmaeli kuvaa vipuli vya dhahabu.)

[25] Wakajibu, “Tutafurahi kuvitoa.” Hivyo
wakatanda vazi chini na kila mwanaume
akatupia juu yake pete kutoka kwenye
fungu lake la nyara. [26] Uzito wa pete
za dhahabu alizoomba zilifikia shekeli
1,700,[h] bila kuhesabu mapambo mengine,
pete za masikio na mavazi ya zambarau
yaliyovaliwa na wafalme wa Midiani, au
mikufu iliyokuwa kwenye shingo za ngamia
zao. [27] [i]Gideoni akatengeneza kisibau kwa
kutumia ile dhahabu, ambacho alikiweka
katika mji wake, yaani, Ofra. Waisraeli
wote wakafanya uasherati kwa kukiabudu
huko, nacho kikawa mtego kwa Gideoni
na jamaa yake.

[28] [j]Hivyo Midiani ikashindwa mbele ya
Israeli nayo haikuinua kichwa chake tena.
Wakati wa siku za uhai wa Gideoni, nchi
ikafurahia amani miaka arobaini.

*Kifo Cha Gideoni*

[29] [k]Yerub-Baali mwana wa Yoashi akarudi
kwenda kuishi katika nyumba yake.
[30] [l]Alikuwa na wana sabini wa kwake
mwenyewe, kwa kuwa alikuwa na wake
wengi. [31] [m]Suria wake, aliyekuwa anaishi
huko Shekemu, pia alimzalia mwana,
ambaye alimwita Abimeleki. [32] [n]Gideoni
mwana wa Yoashi akafa akiwa na umri
mzuri wa uzee, na akazikwa katika kaburi la
Yoashi baba yake huko Ofra ya Waabiezeri.

[33] [o]Mara tu alipofariki Gideoni, Waisraeli
wakarudia hali ya uovu na kufanya uasherati
kwa kuabudu Mabaali. Wakamsimamisha

---

[a]**8:14** Kut 3:16
[b]**8:16** 1Sam 14:12
[c]**8:18** Yos 19:22; Amu 4:6
[d]**8:19** Hes 14:21
[e]**8:21** Za 83:11; Isa 3:18
[f]**8:23** Kut 16:8; Hes 11:20; 1Sam 8:7; 12:12
[g]**8:24** Mwa 35:4; 49:27; 16:11; 25:13
[h]26 Shekeli 1,700 ni sawa na kilo 19.5.
[i]**8:27** Kut 25:4; Amu 17:5; 18:14; Yos 18:23; Kut 10:7; 32:2; Za 106:39
[j]**8:28** Za 83:2; Amu 3:11; 5:31
[k]**8:29** Amu 6:32; 7:1; 6:11
[l]**8:30** Amu 9:2, 5, 18, 24; 12:14; 2Fal 10:1
[m]**8:31** Mwa 22:24; Amu 9:1; 10:1; 2Sam 11:21
[n]**8:32** Mwa 15:15
[o]**8:33** Amu 2:11, 13, 19; 9:4, 27, 46

Baal-Berithi kuwa mungu wao na 34 [a]wala hawakumkumbuka BWANA Mungu wao, aliyewaokoa kutoka mikononi mwa adui zao wote kutoka kila upande. 35 [b]Pia wakashindwa kuitendea mema jamaa ya Yerub-Baali (yaani Gideoni) kwa ajili ya mambo yote mema aliyokuwa amefanya kwa ajili yao.

### *Abimeleki Ajaribu Kuanzisha Ufalme*

9 [c]Siku moja Abimeleki mwana wa Yerub-Baali akaenda kwa ndugu ya mama yake huko Shekemu na kuwaambia yeye na ukoo wote wa mama yake, 2 [d]"Waulizeni watu wote wa Shekemu, 'Lipi lililo bora kwenu: Kutawaliwa na wana wote sabini wa Yerub-Baali, au mtu mmoja peke yake?' Kumbukeni kwamba, mimi ni mfupa wenu nyama yenu hasa."

3 Ndugu za mama yake walipowaeleza watu wote wa Shekemu, wakaelekea kumkubali Abimeleki, kwa kuwa walisema, "Yeye ni ndugu yetu." 4 [e]Wakampa shekeli sabini[f] za fedha kutoka hekalu la Baal-Berithi, naye Abimeleki akaitumia kuajiri watu ovyo wasiojali, wakawa ndio wafuasi wake. 5 [g]Akaenda nyumbani kwa baba yake huko Ofra, na juu ya jiwe moja wakawaua ndugu zake sabini, ambao ni wana wa Yerub-Baali. Lakini Yothamu, mwana mdogo wa wote wa Yerub-Baali, akaokoka kwa kujificha. 6 [h]Ndipo watu wote wa Shekemu na Beth-Milo wakakusanyika pamoja chini ya mti mkubwa wa mwaloni penye nguzo iliyoko Shekemu wakamvika Abimeleki taji kuwa mfalme.

7 [i]Yothamu alipoambiwa hayo, akapanda juu ya kilele cha mlima Gerizimu, akawapazia sauti yake akawaambia, "Nisikilizeni enyi watu wa Shekemu, ili Mungu naye apate kuwasikiliza ninyi. 8 Siku moja miti ilitoka ili kwenda kujitawazia mfalme. Ikauambia mzeituni, 'Wewe uwe mfalme wetu.'

9 "Lakini mzeituni ukaijibu, 'Je, niache kutoa mafuta yangu ambayo kwake miungu na wanadamu huheshimiwa, ili nikawe juu ya miti?'

10 "Kisha miti ikauambia mtini, 'Njoo na uwe mfalme wetu!'

11 "Lakini mtini ukaijibu, 'Je, niache kutoa matunda yangu mazuri na matamu, ili niende nikawe juu ya miti?'

12 "Ndipo miti ikauambia mzabibu, 'Njoo na uwe mfalme wetu.'

13 [j]"Lakini mzabibu ukaijibu, 'Je, niache kutoa divai yangu inayofurahisha miungu na wanadamu ili nikawe juu ya miti?'

14 "Mwishoni miti yote ikauambia mti wa miiba, 'Njoo na uwe mfalme wetu.'

15 [k]"Nao mti wa miiba ukaijibu, 'Kama kweli mnataka niwe mfalme wenu, basi njooni mpate kupumzika chini ya kivuli changu. Lakini kama sivyo, moto na utoke kwenye mti wa miiba ukateketeze mierezi ya Lebanoni!'

16 "Basi ikiwa mmetenda kwa uaminifu na heshima kumfanya Abimeleki kuwa mfalme, na kama mmetendea vyema Yerub-Baali na jamaa yake kama ilivyostahili: 17 [l]kwa kuwa baba yangu aliwapigania ninyi na kuhatarisha nafsi yake na kuwaokoa ninyi kutoka mikononi mwa Wamidiani 18 [m](lakini leo mmeasi dhidi ya jamaa ya baba yangu, na kuwaua wanawe sabini juu ya jiwe moja, nanyi mkamfanya Abimeleki mwana wa mwanamke mtumwa kuwa mfalme juu ya Shekemu, kwa kuwa yeye ni ndugu yenu), 19 nanyi kama basi mmemtendea Yerub-Baali na jamaa yake kwa heshima na uaminifu, basi Abimeleki na awe furaha yenu, nanyi mwe furaha yake pia! 20 Lakini kama sivyo, moto na utoke kwa Abimeleki na uwateketeze, ninyi

---

[a]**8:34** Amu 3:7; Neh 9:17; Za 78:11, 42
[b]**8:35** Amu 6:32; 9:16
[c]**9:1** Amu 8:31; 6:32
[d]**9:2** Mwa 29:14
[e]**9:4** Amu 8:33; 11:3; 1Sam 25:25; 2Nya 13:7; Ay 30:8
[f]4 Shekeli 70 za fedha ni sawa na gramu 800.
[g]**9:5** Amu 8:30; 2Fal 11:2; 2Nya 22:9
[h]**9:6** 2Fal 12:20; Mwa 12:6; Amu 4:11
[i]**9:7** Kum 27:12; Yn 4:20
[j]**9:13** Mwa 14:18; Mhu 2:3; Wim 4:10
[k]**9:15** Isa 30:2; Kum 3:25; 1Fal 5:6; Za 29:5; 92:12; Isa 2:13
[l]**9:17** Amu 12:3; 1Sam 19:5; 28:21; Ay 13:14; Za 119:109
[m]**9:18** Amu 8:30

watu wa Shekemu na Beth-Milo, nao moto
utoke kwenu, watu wa Shekemu na Beth-
Milo umteketeze Abimeleki!”
21 [a]Ndipo Yothamu akakimbia, akatoroka
akaenda Beeri, akaishi huko, kwa sababu
alimwogopa ndugu yake Abimeleki.
22 Baada ya Abimeleki kutawala Israeli
kwa muda wa miaka mitatu, 23 [b]Mungu
akaruhusu roho mbaya kati ya Abimeleki na
watu wa Shekemu, nao watu wa Shekemu
wakamtendea Abimeleki kwa hila. 24 [c]Hili
lilitokea ili ule ukatili waliotendewa hao
wana sabini wa Yerub-Baali upatilizwe,
na damu yao iwe juu ya Abimeleki ndugu
yao aliyewaua, na pia iwe juu ya watu
wa Shekemu, ambao walimsaidia kuua
ndugu zake. 25 Hivyo, kutokana na uadui
juu yake watu wa Shekemu wakaweka
watu wa kumvizia katika vilele vya milima.
Wakawanyang’anya watu wote waliopita
karibu nao, nayo haya yakaarifiwa kwa
Abimeleki.
26 Basi Gaali mwana wa Ebedi akaenda
pamoja na ndugu zake wakaingia Shekemu,
nao watu wa huko wakamtumainia yeye.
27 [d]Wakaenda mashambani mwao kuvuna
zabibu na kuzisindika hizo zabibu,
wakafanya sikukuu katika hekalu la
mungu wao. Wakati wakila na kunywa,
wakamlaani Abimeleki. 28 [e]Gaali mwana
wa Ebedi akasema, “Abimeleki ni nani, na
Shekemu ni nani, hata tumtumikie? Je,
yeye si mwana wa Yerub-Baali? Naye Zebuli
si ndiye msaidizi wake? Basi watumikieni
watu wa Hamori, babaye Shekemu. Kwa
nini tumtumikie Abimeleki? 29 [f]Laiti watu
hawa wangekuwa chini ya amri yangu!
Basi mimi ningemwondoa huyo Abimeleki.
Ningemwambia Abimeleki, ‘Ondoa jeshi
lako lote.’ ”
30 Zebuli aliyekuwa mtawala wa mji
aliposikia aliyosema Gaali mwana wa
Ebedi, akakasirika sana. 31 Akatuma ujumbe
uende kwa Abimeleki kwa siri na kusema,
“Gaali mwana wa Ebedi na ndugu zake
wamekuja Shekemu, na wanauchochea mji
huu kinyume chako. 32 [g]Sasa, basi, usiku
huu wewe uondoke na watu wako ili mje
kuwavizia mashambani. 33 [h]Kisha asubuhi
wakati wa kuchomoza jua, amka mapema
na ujipange dhidi ya huo mji. Wakati yeye
na jeshi lililo pamoja naye watakapotoka
kukabiliana nanyi, mwaweza kuwatendea
kwa kadiri mnavyoweza.”
34 Kwa hiyo Abimeleki pamoja na jeshi
lake lote wakaondoka usiku na kujificha
karibu na Shekemu wakiwa vikosi vinne.
35 [i]Basi Gaali mwana wa Ebedi alikuwa
ametoka nje akawa amesimama katika
ingilio la mji wakati ule ule ambao
Abimeleki na watu wake walipokuwa
wanatoka sehemu zao za maficho.
36 Gaali alipowaona, akamwambia Zebuli,
“Tazama, watu wanashuka kutoka kwenye
vilele vya milima!”
Zebuli akajibu, “Wewe unaona vivuli vya
milima kana kwamba ni watu.”
37 Lakini Gaali akasema tena, “Tazama,
watu wanashuka kutoka katikati ya nchi
na kikosi kimoja kinakuja kutoka Tabur-
Ezeri na kikosi kingine kutoka upande wa
Elon-Meonenimu.”
38 Ndipo Zebuli akamwambia, “Kuko
wapi kujivuna kwako sasa, wewe uliyesema,
‘Huyo Abimeleki ni nani hata tumtumikie?’
Hawa si wale watu uliowadharau? Toka nje
sasa ukapigane nao!”
39 Basi Gaali akatoka akawaongoza watu
wa Shekemu kupigana na Abimeleki.
40 Abimeleki akamfukuza, watu wengi
wakajeruhiwa katika kukimbia huko,
njia nzima hadi kwenye ingilio la lango.
41 Abimeleki akakaa Aruma, naye Zebuli
akawafukuza Gaali na ndugu zake watoke
Shekemu.
42 Kesho yake watu wa Shekemu wakatoka
wakaenda mashambani, Abimeleki

[a]**9:21** Hes 21:16
[b]**9:23** 1Sam 16:14; 18:10; 19:9; 1Fal 22:22
[c]**9:24** Amu 8:30; Mwa 9; 6; Hes 35:33; 1Fal 2:32; Kum 27:25
[d]**9:27** Isa 16:10; Amo 5:11; 9:13; Amu 8:33
[e]**9:28** 1Sam 25:10; 1Fal 12:16; Mwa 33:19; 34:2-6
[f]**9:29** 2Sam 15; 4
[g]**9:32** Yos 8:2
[h]**9:33** 1Sam 10:7
[i]**9:35** Yos 2:5; Za 32:7; Isa 28:15-17; Yer 49:10

akaambiwa juu ya jambo hili. 43 [a]Hivyo
akawachukua watu wake, akawagawanya
katika vikosi vitatu na kuwaweka waviziao
huko mashambani. Alipowaona watu
wanatoka kwenda nje ya mji, akainuka
dhidi yao na kuwashambulia. 44 Abimeleki
pamoja na vile vikosi wakaharakisha
kwenda mbele kwenye nafasi, mahali pa
ingilio la lango la mji. Vile vikosi viwili
vikawawahi wale waliokuwa mashambani
na kuwaua. 45 [b]Siku hiyo nzima Abimeleki
akazidisha mashambulizi yake dhidi ya
mji hadi akawa ameuteka na kuwaua watu
wa huo mji. Kisha akauangamiza mji na
kusambaza chumvi juu yake.

46 [c]Kwa kusikia jambo hili watu
wote katika mnara wa Shekemu,
wakaingia kwenye ngome ya hekalu la
El-Berithi. 47 Abimeleki aliposikia kuwa
wamekusanyika huko, 48 [d]yeye na watu
wake wote wakakwea kwenye Mlima
Salmoni. Abimeleki akachukua shoka,
akakata baadhi ya matawi, ambayo
aliyachukua mabegani. Akawaagiza wale
watu waliokuwa pamoja naye kuwa,
“Fanyeni kile mlichoona mimi nikifanya!”
49 Basi watu wote wakakata matawi na
kumfuata Abimeleki. Wakayakusanya hayo
matawi juu ya ngome na kuitia moto ili
kuwachoma wale watu wote waliokuwa
ndani yake. Hivyo watu wote katika mnara
wa Shekemu, karibia watu 1,000 waume
kwa wake, pia wakafa.

50 [e]Baadaye Abimeleki akaenda Thebesi
na kuuzingira kwa jeshi na kuuteka.
51 Hata hivyo, ndani ya huo mji kulikuwa
na mnara imara, ambako watu wote wa
mji wanaume na wanawake, watu wote wa
mji, walikimbilia ndani yake. Wakajifungia
ndani yake na kupanda juu ya paa la mnara.
52 Abimeleki akaja kwenye ule mnara na
kuushambulia, lakini alipokaribia kwenye
ingilio la mnara ili kuuchoma kwa moto,
53 [f]mwanamke mmoja akaangusha sehemu
ya juu ya jiwe la kusagia juu ya kichwa cha
Abimeleki, likapasua fuvu la kichwa chake.

54 [g]Akamwita kwa haraka kijana yule
aliyechukua silaha zake, na kumwambia,
“Chukua upanga wako na uniue, watu
wasije wakasema kwamba, ‘Mwanamke
amemuua.’ ” Basi yule kijana akamchoma
upanga, naye akafa. 55 Waisraeli walipoona
kuwa Abimeleki amekufa, kila mtu akaenda
nyumbani kwake.

56 Hivyo ndivyo Mungu alivyolipiza uovu
ule ambao Abimeleki alikuwa ameutenda
kwa baba yake kwa kuwaua ndugu zake
sabini. 57 [h]Mungu akawapatiliza watu wa
Shekemu uovu wao juu ya vichwa vyao,
na juu yao ikaja laana ya Yothamu mwana
wa Yerub-Baali.

### *Tola*

10 [i]Baada ya Abimeleki, Tola mwana wa
Pua mwana wa Dodo, mtu wa Isakari,
aliyeishi huko Shamiri, katika nchi ya
vilima ya Efraimu, akainuka kuokoa Israeli.
2 Akaamua Israeli kwa miaka ishirini na
mitatu. Ndipo akafa, naye akazikwa huko
Shamiri.

### *Yairi*

3 [j]Baada yake akafuatiwa na Yairi,
Mgileadi, ambaye aliamua Israeli kwa
miaka ishirini na miwili. 4 [k]Alikuwa na wana
thelathini waliopanda punda thelathini.
Nao walikuwa na miji thelathini iliyoko
Gileadi, inayoitwa Hawoth-Yairi mpaka leo.
5 [l]Yairi akafa, naye akazikwa huko Kamoni.

### *Yefta*

6 [m]Wana wa Israeli wakatenda tena
maovu machoni pa Bwana. Wakaabudu
Mabaali na Maashtorethi, miungu ya

[a]**9:43** Amu 7:16; Yos 8:2
[b]**9:45** Yer 48:9
[c]**9:46** Amu 8:33
[d]**9:48** Za 68:14
[e]**9:50** 2Sam 11:21
[f]**9:53** 2Sam 11:21
[g]**9:54** 1Sam 31:4; 2Sam 1:9
[h]**9:57** Za 94:23
[i]**10:1** Amu 8:31; Mwa 30:18; 46:13; Amu 6:14; Yos 15:48; Amu 2:16
[j]**10:3** Hes 32:41
[k]**10:4** Mwa 49:11; 1Fal 1:33; Hes 32:41
[l]**10:5** Hes 32:41
[m]**10:6** Amu 2:11, 13; Eze 27:16; Mwa 10:15; 19:38; Hes 21:29; Mwa 26:1; Amu 2:12; Kum 32:15

Aramu, miungu ya Sidoni, miungu ya
Moabu, miungu ya Waamoni na miungu ya
Wafilisti. Kwa kuwa Waisraeli walimwacha
BWANA wala hawakuendelea kumtumikia,
7 [a]hivyo hasira ya BWANA ikawaka dhidi
ya Israeli, naye akawatia mikononi mwa
Wafilisti na Waamoni, 8 [b]ambao waliwaonea
na kuwatesa mwaka ule. Kwa miaka kumi
na minane wakawatesa Waisraeli wote
upande wa mashariki ya Mto Yordani katika
Gileadi, nchi ya Waamori. 9 [c]Waamoni nao
wakavuka Yordani ili kupigana na Yuda,
Benyamini na nyumba ya Efraimu, nayo
nyumba ya Israeli ikawa katika taabu
kubwa. 10 [d]Ndipo Waisraeli wakamlilia
BWANA wakasema, "Tumetenda dhambi
dhidi yako, kumwacha Mungu wetu na
kutumikia Mabaali."

11 [e]BWANA akawaambia, "Wakati
Wamisri, Waamori, Waamoni, Wafilisti,
12 [f]Wasidoni, Waamaleki na Wamaoni
walipowaonea na ninyi mkanililia na
kuomba msaada, je, sikuwaokoa kutoka
mikononi mwao? 13 [g]Lakini ninyi mmeniacha
mimi na kutumikia miungu mingine, kwa
hiyo sitawaokoa tena. 14 [h]Nendeni mkaililie
ile miungu mlioichagua. Hiyo miungu na
iwaokoe mnapokuwa katika taabu!"

15 [i]Lakini Waisraeli wakamwambia
BWANA, "Tumetenda dhambi. Ututendee
lile unaloona kuwa jema kwako, lakini
twakusihi utuokoe sasa." 16 [j]Nao wakaiondoa
hiyo miungu migeni katikati yao nao
wakamtumikia BWANA. Naye akahuzunika
kwa sababu ya taabu ya Israeli.

17 [k]Ndipo Waamoni wakaitwa vitani
na kupiga kambi huko Gileadi, Waisraeli
wakakusanyika na kupiga kambi huko
Mispa. 18 [l]Viongozi wa watu wa Gileadi
wakaambiana wao kwa wao, "Yeyote
yule atakayeanzisha mashambulizi dhidi
ya Waamoni atakuwa kiongozi wa wote
wakaao Gileadi."

11 [m]Basi Yefta Mgileadi alikuwa mtu
shujaa. Baba yake alikuwa Gileadi,
naye mama yake alikuwa kahaba. 2 Mke
wa Gileadi akamzalia wana wengine, nao
watoto hao walipokua, wakamfukuza Yefta
na kumwambia, "Wewe huwezi kupata
urithi katika jamii yetu, kwa sababu wewe
ni mwana wa mwanamke mwingine." 3 [n]Basi
Yefta akawakimbia ndugu zake akaenda
kuishi katika nchi ya Tobu, mahali ambako
watu waasi walijiunga naye na kumfuata.

4 [o]Baada ya muda Waamoni wakafanya
vita na Israeli, 5 viongozi wa Gileadi
wakaenda kumchukua Yefta katika nchi
ya Tobu. 6 Wakamwambia Yefta, "Uwe
jemadari wetu, ili tuweze kupigana na
Waamoni."

7 [p]Yefta akawaambia, "Je, hamkunichukia
mimi na kunifukuza katika nyumba ya baba
yangu? Kwa nini mnanijia sasa, wakati mna
matatizo."

8 [q]Viongozi wa Gileadi wakamwambia
Yefta, "Lakini sasa tumegeuka kukuelekea
wewe, ili uende pamoja nasi kupigana na
Waamoni, nawe utakuwa kiongozi wetu
juu ya watu wote wa Gileadi."

9 Yefta akawaambia, "Ikiwa mtanirudisha
kwetu kupigana na Waamoni, naye BWANA
akanisaidia kuwashinda, Je, ni kweli
nitakuwa kiongozi wenu?"

10 [r]Viongozi wa Gileadi wakamjibu Yefta,
"BWANA ndiye shahidi yetu. Kwa hakika

[a]**10:7** Kum 31:17; 32:30
[b]**10:8** Yos 12:2
[c]**10:9** Amu 1:22; 11:4
[d]**10:10** Amu 3:9; Kut 9:27; Za 32:5; Yer 3:25; 8:14; 14:20; 2:27
[e]**10:11** Kut 14:30; Mwa 14:7; Amu 3:13, 31
[f]**10:12** Mwa 14:7; Yos 15:55; Amu 4:3; Za 106:42
[g]**10:13** Kum 32:15; Yer 11:10; 13:10
[h]**10:14** Isa 44:17; 57:13; Kum 32:37; Yer 2:28; 11:12; Hab 2:18
[i]**10:15** 1Sam 3:18; 2Sam 10:12; 15:26; Ay 1:21; Isa 39:8
[j]**10:16** Yos 24:23; Yer 18:8; Isa 63:9; Kum 32:36; Za 106:44-45
[k]**10:17** Mwa 31:49; Amu 11:29
[l]**10:18** Amu 11:8-9
[m]**11:1** Amu 12:1; 1Sam 12:11; Ebr 11:32; Amu 6:12; Hes 26:29; Mwa 38; 15
[n]**11:3** 2Sam 10:6-8; Amu 9:4
[o]**11:4** Amu 10:9
[p]**11:7** Mwa 26:16, 27
[q]**11:8** Amu 10:18
[r]**11:10** Mwa 31:50; Isa 1:2; Yer 42:5

tutafanya kama usemavyo.” 11 [a]Basi Yefta
akaenda na viongozi wa Gileadi, nao watu
wakamfanya kiongozi na jemadari wao.
Naye akarudia maneno yake yote mbele
za BWANA huko Mispa.
12 Ndipo Yefta akatuma wajumbe kwa
mfalme wa Waamoni akisema, “Una nini
juu yetu, hata umekuja kushambulia nchi
yetu?”
13 [b]Mfalme wa Waamoni akawajibu
wajumbe wale wa Yefta, “Wakati Waisraeli
walipopanda kutoka Misri, waliichukua
nchi yangu kuanzia Arnoni mpaka Yaboki,
hadi kufikia Yordani. Sasa rudisha kwa
amani.”
14 Yefta akarudisha wajumbe kwa mfalme
wa Waamoni, 15 [c]kusema:

“Hili ndilo asemalo Yefta, Israeli
hawakuchukua nchi ya Moabu wala
ya Waamoni. 16 [d]Lakini walipopanda
kutoka Misri, Israeli walipitia katika
jangwa hadi Bahari ya Shamu na
wakafika Kadeshi. 17 [e]Ndipo Israeli
wakatuma wajumbe kwa mfalme wa
Edomu, wakisema, ‘Tupe ruhusa kupita
katika nchi yako,’ Lakini mfalme wa
Edomu hakutusikia. Wakapeleka pia
wajumbe kwa mfalme wa Moabu, naye
akakataa. Kwa hiyo Israeli wakakaa
huko Kadeshi.
18 [f]“Baadaye wakasafiri kupitia
jangwa, wakiambaa na nchi za
Edomu na Moabu, wakapitia upande
wa mashariki wa nchi ya Moabu na
kupiga kambi upande mwingine wa
Arnoni. Hawakuingia katika nchi ya
Moabu, kwa kuwa Arnoni ilikuwa
mpaka wake.
19 [g]“Kisha Israeli wakatuma wajumbe
kwa Sihoni mfalme wa Waamori,
aliyetawala Heshboni, na kumwambia,
‘Tupe ruhusa kupita katika nchi yako
ili kufikia mahali petu.’ 20 [h]Hata hivyo,
Sihoni hakuwaamini Waisraeli kupita
katika nchi yake. Akaandaa jeshi lake
lote na kupiga kambi huko Yahasa, nao
wakapigana na Israeli.
21 “Ndipo BWANA, Mungu wa
Israeli, akamtia Sihoni na watu wake
wote mikononi mwa Israeli, nao
wakawashinda. Israeli wakaitwaa nchi
yote ya Waamori, waliokuwa wakiishi
katika nchi hiyo, 22 [i]wakiiteka nchi
yote kuanzia Arnoni mpaka Yaboki,
na kutoka jangwani mpaka Yordani.
23 “Basi kwa kuwa BWANA, Mungu
wa Israeli, amewafukuza Waamori
watoke mbele ya watu wake Israeli,
wewe unayo haki gani ya kuitamalaki?
24 [j]Je, haikupasi kuchukua kile ambacho
mungu wako Kemoshi amekupa? Vivyo
hivyo, chochote kile BWANA Mungu
wetu alichotupa sisi, tutakimiliki.
25 [k]Je, wewe ni bora kuliko Balaki
mwana wa Sipori, mfalme wa Moabu?
Je, yeye alishagombana na Israeli au
kupigana nao wakati wowote? 26 [l]Kwa
maana kwa miaka 300 Israeli wameishi
Heshboni na vijiji vyake, Aroeri na
vijiji vyake, na katika miji yote iliyo
kando ya Arnoni. Kwa nini wewe
haukuyachukua wakati huo? 27 [m]Mimi
sijakukosea jambo lolote, bali wewe
ndiye unayenikosea kwa kufanya vita
nami. Basi BWANA, aliye Mwamuzi,
leo na aamue ugomvi kati ya Waisraeli
na Waamoni.”

28 Hata hivyo, Mfalme wa Waamoni,
hakuyajali maneno ya ujumbe wa Yefta.
29 [n]Ndipo Roho wa BWANA akaja juu

---

[a]**11:11** 1Sam 9:4; 2Sam 3:17; Kut 19:9; 1Sam 8; 21; Yos 11:3
[b]**11:13** Hes 21:13; 21:24; Mwa 32:22
[c]**11:15** Kum 2:9; 1:19
[d]**11:16** Hes 14:25; Kum 1:40; Mwa 14:7; Hes 20:1
[e]**11:17** Mwa 32:3; Hes 20:14-17; Yer 48:1; Yos 24:9
[f]**11:18** Hes 20:21; Kum 2:8; Hes 21:13; 21:4
[g]**11:19** Hes 21:21-22; Yos 12:2; Kum 2:26-27
[h]**11:20** Hes 21:23; Kum 2:32
[i]**11:22** Hes 21:21-22; Kum 2:36
[j]**11:24** Hes 21:29; Yos 3:10; Kum 2:3; 1Fal 11:7
[k]**11:25** Hes 22:2; Yos 24:9
[l]**11:26** Hes 21:25; 32:34; Yos 13:9
[m]**11:27** Mwa 18:25; 16:5; 2Nya 20; 12; Mwa 31:53; 1Sam 24:12-15
[n]**11:29** Amu 3:10; Mwa 31:49; Amu 10:17; Hes 11:25; Isa 11; 2

ya Yefta. Akapita katikati ya Gileadi na Manase, pia akapita katika Mispa ya Gileadi, na kutokea huko akasonga mbele kushambulia Waamoni. 30 [a]Naye Yefta akaweka nadhiri mbele za BWANA akisema, "Ikiwa utawatia Waamoni mikononi mwangu, 31 [b]chochote kile kitakachotoka katika mlango wa nyumba yangu cha kwanza ili kunilaki nirudipo kwa amani katika kuwashinda Waamoni, kitakuwa ni cha BWANA na nitakitoa kuwa sadaka ya kuteketezwa."

32 Ndipo Yefta akavuka kupigana na hao Waamoni, naye BWANA akawatia mkononi mwake. 33 [c]Akawapiga kwa ushindi mkubwa kuanzia Aroeri mpaka karibu na Minithi na kuendelea mpaka Abel-Keramimu, miji yote iliyopigwa ni ishirini. Basi Israeli wakawashinda Waamoni.

34 [d]Yefta aliporudi nyumbani Mispa, tazama, binti yake akatoka ili kumlaki kwa matari na kucheza. Alikuwa ndiye mtoto pekee, hakuwa na mwana wala binti mwingine. 35 [e]Alipomwona akararua mavazi yake akalia, "Ee! Binti yangu! Umenifanya niwe na huzuni na kunyong'onyea sana, kwa kuwa nimeweka nadhiri kwa BWANA, ambayo siwezi kuivunja."

36 [f]Akajibu, "Baba yangu, umetoa neno lako kwa BWANA. Nitendee mimi kama vile ulivyoahidi, kwa kuwa BWANA amekupa ushindi dhidi ya adui zako Waamoni." 37 Naye akamwambia baba yake, "Naomba nifanyiwe jambo hili. Nipewe miezi miwili ili kuzunguka vilimani nikaulilie ubikira wangu, mimi na wenzangu."

38 Baba yake akamwambia, "Waweza kwenda." Naye akamwacha aende kwa miezi miwili. Hivyo akaondoka pamoja na wasichana wenzake, naye akaulilia ubikira wake huko vilimani kwa sababu asingeolewa kamwe. 39 Baada ya hiyo miezi miwili, alirejea kwa baba yake, naye baba yake akamtendea kama alivyokuwa ametoa nadhiri yake. Naye alikuwa bikira.

Nayo ikawa desturi katika Israeli, 40 kwamba kila mwaka binti wa Israeli huenda kwa siku nne ili kumkumbuka huyo binti wa Yefta, Mgileadi.

### *Yefta Na Efraimu*

12 [g]Watu wa Efraimu wakaita majeshi yao, wakavuka kwenda Zafoni, wakamwambia Yefta, "Kwa nini mmekwenda kupigana na Waamoni bila kutuita ili twende pamoja nawe? Basi tutaichoma moto nyumba yako, pamoja nawe ukiwa ndani yake."

2 Yefta akajibu, "Mimi na watu wangu tulikuwa na ugomvi mkubwa na Waamoni, hata ingawa niliwaita hamkuniokoa katika mkono wao. 3 [h]Nilipoona kuwa hamkunipa msaada nikauhatarisha uhai wangu na nikavuka kupigana na Waamoni. Naye BWANA akanipatia ushindi dhidi yao. Sasa kwa nini mnanijia leo ili kupigana nami?"

4 [i]Ndipo Yefta akakusanya watu wa Gileadi pamoja na kupigana na Efraimu. Wagileadi wakawashinda Efraimu, kwa kuwa Waefraimu walisema, "Ninyi Wagileadi ni watoro mliotoroka toka Efraimu na Manase." 5 [j]Wagileadi wakaviteka vivuko vya Yordani dhidi ya hao Waefraimu, kisha ilikuwa yeyote yule aliyenusurika katika Efraimu aliposema, "Niache nivuke," hao watu wa Gileadi walimuuliza, "Je wewe ni Mwefraimu?" Kama alijibu "Hapana," 6 walimwambia, "Sawa, sema 'Shibolethi.' " Iwapo alitamka, "Sibolethi," kwa sababu hakuweza kutamka hilo neno sawasawa, walimkamata na kumuua hapo kwenye vivuko vya Yordani. Waefraimu 42,000 waliuawa wakati huo.

7 Yefta akawa mwamuzi wa Waisraeli kwa muda wa miaka sita. Basi Yefta akafa, akazikwa katika mmojawapo wa miji ya Gileadi.

---

[a]**11:30** Mwa 28:20; Hes 30:10; 1Sam 1:11; Mit 31:2
[b]**11:31** Mwa 28:21; 8:20; Law 1:3; Amu 13:16
[c]**11:33** Eze 27:17
[d]**11:34** Kut 15:20; Mwa 31:27; Yer 31:4; Zek 12; 10
[e]**11:35** Hes 14:6; 30:2; Kum 23:21; Mhu 5:2-5
[f]**11:36** Lk 1:38; Hes 31:3; 2Sam 18:19

[g]**12:1** Yos 13:27; Amu 11:1; 8:1
[h]**12:3** Amu 9:17; Kum 20:7; 1Sam 19:5; Ay 13:14
[i]**12:4** 1Fal 17:1; Mwa 46:20; Isa 9:21; 19:2
[j]**12:5** Yos 2:5-7; Amu 3:28

*Ibzani, Eloni Na Abdoni*

8 [a]Baada yake, Ibzani wa Bethlehemu
akawa mwamuzi wa Israeli. 9 Alikuwa
na wana thelathini na binti thelathini.
Akawaoza binti zake kwa watu wengine
nje ya ukoo wake, na kuwatwalia wanawe
wanawake thelathini toka nje ya ukoo
wake. Ibzani akawa mwamuzi wa Israeli
kwa muda wa miaka saba. 10 Ibzani akafa,
akazikwa huko Bethlehemu.
11 Baada yake Eloni, Mzabuloni, akawa
mwamuzi wa Israeli, naye akawaamua kwa
muda wa miaka kumi. 12 [b]Kisha Eloni akafa,
akazikwa katika Aiyaloni, katika nchi ya
Zabuloni.
13 [c]Baada yake, Abdoni mwana wa Hileli,
Mpirathoni, akawa mwamuzi wa Israeli.
14 [d]Naye akazaa wana arobaini na wana
wa wanawe thelathini waliopanda punda
sabini. Akawa mwamuzi wa Israeli kwa
muda wa miaka minane. 15 [e]Ndipo Abdoni
mwana wa Hileli, Mpirathoni, akafa, naye
akazikwa huko Pirathoni katika Efraimu,
katika nchi ya vilima ya Waamaleki.

*Kuzaliwa Kwa Samsoni*

13 [f]Waisraeli wakafanya maovu tena
mbele za BWANA. Hivyo BWANA
akawatia mikononi mwa Wafilisti kwa
muda wa miaka arobaini.
2 [g]Basi palikuwa na mtu mmoja wa Sora,
aliyeitwa Manoa, wa kabila la Wadani,
naye alikuwa na mke ambaye alikuwa
tasa na hakuwa na mtoto. 3 [h]Malaika wa
BWANA akamtokea huyo mwanamke
na kumwambia, "Wewe ni tasa na huna
mtoto, lakini utachukua mimba na utamzaa
mtoto mwanaume. 4 [i]Lakini ujihadhari
sana usinywe mvinyo wala kileo kingine
chochote, wala usile kitu chochote kilicho
najisi, 5 [j]kwa kuwa utachukua mimba na
utamzaa mtoto mwanaume. Wembe usipite
kichwani pake, kwa kuwa huyo mwana
atakuwa Mnadhiri wa Mungu, aliyewekwa
wakfu kwa ajili ya Mungu tangu tumboni
mwa mama yake, naye ataanza kuwaokoa
Waisraeli kutoka mikononi mwa Wafilisti."
6 [k]Ndipo huyo mwanamke akamwendea
mumewe na kumweleza kuwa, "Mtu wa
Mungu alinijia. Kule kuonekana kwake
kulikuwa kama kwa malaika wa Mungu,
wa kutisha sana. Sikumuuliza alikotoka
wala hakuniambia jina lake. 7 [l]Lakini
aliniambia, 'Utachukua mimba na utazaa
mtoto mwanaume. Basi sasa, usinywe
mvinyo wala kileo kingine chochote wala
usile kitu kilicho najisi, kwa kuwa huyo
mtoto atakuwa Mnadhiri wa Mungu tangu
tumboni mwa mama yake mpaka kufa
kwake.' "
8 Ndipo Manoa akamwomba BWANA,
akasema: "Ee Bwana, nakusihi, huyo mtu
wa Mungu uliyemtuma kwetu aje tena ili
atufundishe jinsi ya kumlea huyo mwana
atakayezaliwa."
9 Mungu akamsikia Manoa, naye malaika
wa Mungu akamjia tena huyo mwanamke
alipokuwa shambani, lakini mumewe
Manoa hakuwepo. 10 Basi yule mwanamke
akaenda haraka na kumwambia mumewe,
"Tazama mtu yule aliyenitokea siku ile
yupo hapa!"
11 Manoa akainuka akaandamana na
mkewe. Alipomfikia yule mtu akamuuliza,
"Je, wewe ndiye yule uliyesema na mke
wangu?"
Akasema, "Mimi ndiye."
12 Basi Manoa akamuuliza, "Wakati
maneno yako yatakapotimia, masharti ya
maisha ya mtoto huyu yatakuwa nini na
kazi yake itakuwa ni nini?"
13 Malaika wa BWANA akamjibu,
"Mke wako hana budi kufanya yale yote
niliyomwambia. 14 [m]Kamwe asile kitu

[a]**12:8** Mwa 35:19
[b]**12:12** Yos 10:12
[c]**12:13** 2Sam 23:30; 1Nya 11:31; 27:14
[d]**12:14** Amu 8:30; 5:10; 10:4
[e]**12:15** Amu 5:14
[f]**13:1** Amu 3:4, 31; 14:4; 1Sam 12:9
[g]**13:2** Yos 15:33; Amu 16:31; Mwa 30:6; 11:30
[h]**13:3** Mwa 16:7; Isa 7:14; Lk 1:13; Amu 6:12
[i]**13:4** Law 10:9; Hes 6:2-4; Lk 1:15
[j]**13:5** Mwa 3:15; 1Sam 1:11; 7:13; Hes 6:2, 13; Amo 2:11-12
[k]**13:6** 1Sam 2:27; 9:6; 1Fal 13:1; 17:18; Hes 22:22; Za 66:5; Mt 28:3
[l]**13:7** Yer 35:6; Law 10:6; 1Sam 1:11, 28
[m]**13:14** Law 10:9; Hes 6:4

chochote kitakachotoka katika mzabibu,
wala asinywe mvinyo wa aina yoyote wala
kileo chochote wala asile kitu chochote
kilicho najisi. Hana budi kufanya kila kitu
nilichomwagiza.”
15 [a]Manoa akamjibu yule malaika wa
Bwana, “Twakuomba usubiri kwanza ili
tuweze kuandaa mwana-mbuzi kwa ajili
yako.”
16 [b]Malaika wa Bwana akamjibu,
“Hata kama utanizuia, sitakula chochote
kwako. Lakini ukitaka kuandaa sadaka ya
kuteketezwa, mtolee Bwana hiyo sadaka.”
(Kwa kuwa Manoa hakujua kuwa alikuwa
malaika wa Bwana.)
17 [c]Ndipo Manoa akamuuliza yule
malaika wa Bwana, “Jina lako ni nani, ili
kwamba tuweze kukupa heshima hapo hayo
uliyonena yatakapotimia?”
18 Akamjibu, “Kwa nini unauliza Jina
langu? Ni Jina la ajabu.” 19 [d]Ndipo Manoa
akamchukua mwana-mbuzi, pamoja na
sadaka ya unga, naye akamtolea Bwana
dhabihu hapo juu ya mwamba. Naye yule
malaika wa Bwana akafanya jambo la
ajabu wakati Manoa na mkewe wakiwa
wanaangalia: 20 [e]Mwali wa moto kutoka
hapo madhabahuni ulipowaka kuelekea
mbinguni, malaika wa Bwana akapaa ndani
ya huo mwali. Manoa na mkewe, kwa kuona
jambo hili, wakaanguka chini kifudifudi.
21 [f]Malaika wa Bwana hakumtokea tena
Manoa na mkewe. Ndipo Manoa akatambua
kuwa huyo alikuwa malaika wa Bwana.
22 [g]Manoa akamwambia mkewe, “Hakika
tutakufa, kwa kuwa tumemwona Mungu.”
23 [h]Lakini mkewe akamwambia, “Ikiwa
Bwana alikuwa amekusudia kutuua,
asingelipokea sadaka ya kuteketezwa na
sadaka ya unga kutoka mikononi mwetu,
wala asingelituonyesha mambo haya yote
wala kututangazia mambo kama haya
wakati huu.”
24 [i]Yule mwanamke akazaa mtoto wa
kiume akamwita jina lake Samsoni. Kijana
akakua, naye Bwana akambariki. 25 [j]Roho
wa Bwana akaanza kumsukuma wakati
alipokuwa huko Mahane-Dani, kati ya Sora
na Eshtaoli.

*Ndoa Ya Samsoni*

14 [k]Samsoni akateremkia Timna,
akamwona mwanamke wa Kifilisti.
2 [l]Alipopanda kutoka huko, akawaambia
baba yake na mama yake, “Nimemwona
mwanamke wa Kifilisti huko Timna; basi
mnipe ili awe mke wangu.”
3 [m]Baba yake na mama yake wakamjibu,
“Je, hakuna mwanamke miongoni mwa
jamaa yako au miongoni mwa ndugu
zako, hata ulazimike kwenda kujitwalia
mwanamke kutoka kwa hawa Wafilisti
wasiotahiriwa?”
Lakini Samsoni akamwambia baba
yake, “Nipatieni huyo kwa maana ndiye
alinipendeza.” 4 [n](Baba yake na mama yake
hawakujua kuwa jambo hili limetoka kwa
Bwana, kwani alikuwa akitafuta sababu ya
kukabiliana na Wafilisti; kwa kuwa wakati
huo walikuwa wakiwatawala Waisraeli.)
5 Samsoni akateremkia Timna pamoja
na baba yake na mama yake. Walipofika
kwenye mashamba ya mizabibu huko
Timna, ghafula mwana simba akamjia
akimngurumia. 6 [o]Roho wa Bwana akaja
juu yake kwa nguvu, naye akampasua
yule simba kwa mikono yake bila silaha
yoyote kama vile mtu ampasuavyo mwana-
mbuzi, wala hakumwambia baba yake wala
mama yake aliyoyafanya. 7 Basi akateremka

[a] **13:15** Amu 9:16
[b] **13:16** Amu 11:31; 6:22
[c] **13:17** Mwa 32:29; Isa 9:6
[d] **13:19** Amu 6:20
[e] **13:20** Law 9:24; Mwa 17:4; Eze 1:28; Mt 17:6
[f] **13:21** Amu 6:22
[g] **13:22** Hes 17:12; Kum 5:26; Mwa 16:13; Kut 3:6; 24:10; Amu 6:22
[h] **13:23** Za 25:14
[i] **13:24** Amu 14:1; 15:1; 16:1; Ebr 11:32; 1Sam 2:21-26; 3:19; Lk 1:80
[j] **13:25** Amu 3:10; 18:12
[k] **14:1** Amu 13:24; Mwa 38:12
[l] **14:2** Mwa 21:21; 34:4
[m] **14:3** Mwa 24:4; 34:14; 1Sam 14:6; Kut 34:16; Kum 7:3
[n] **14:4** Kum 2:30; Yos 11:20; Amu 13:1; 15:11
[o] **14:6** Amu 3:10; 1Sam 17:35; Amu 13:25

na kuongea na yule mwanamke, naye
akampendeza Samsoni.
8 Baada ya muda aliporudi ili akamwoe,
akatazama kando ili kuutazama mzoga
wa yule simba, na tazama, kulikuwa na
kundi la nyuki ndani ya ule mzoga wa
simba na kulikuwa na asali; 9 akachukua
asali mkononi mwake akaendelea huku
akila. Alipowafikia baba yake na mama
yake, akawapa ile asali nao wakala. Lakini
hakuwaambia kuwa alitwaa asali kutoka
kwenye mzoga wa simba.
10 [a]Basi baba yake akateremka kumwona
huyo mwanamke. Samsoni akafanya
karamu huko, kama ilivyokuwa desturi ya
vijana. 11 Watu walipomwona, wakaleta
vijana wenzake thelathini ili kuwa pamoja
naye.
12 [b]Samsoni akawaambia, "Niwape
kitendawili, mkiweza kunipa jibu katika
muda wa siku hizi saba za karamu,
nitawapa mavazi thelathini ya kitani na
mavazi mengine mivao thelathini. 13 Lakini
msipoweza kufumbua, ndipo ninyi mtanipa
mavazi thelathini ya kitani na mavazi
mengine mivao thelathini."

Wakamwambia, "Tuambie hicho
kitendawili, hebu na tukisikie."
14 Akawaambia,

"Ndani ya mlaji,
kulitoka kitu cha kuliwa,
ndani ya mwenye nguvu,
kulitoka kitu kitamu."

Kwa muda wa siku tatu hawakuweza kutoa
jibu.
15 [c]Siku ya saba, wakamwambia mkewe
Samsoni, "Mbembeleze mumeo ili atueleze
hicho kitendawili, la sivyo tutakuchoma
moto wewe na wa nyumba ya baba yako.
Je, mmetualika ili mpate kutunyang'anya
kile tulicho nacho?"
16 [d]Basi mke wa Samsoni akalia mbele
yake na kumwambia, "Unanichukia!
Hunipendi kabisa. Umewategea watu wangu
kitendawili, lakini mimi hujaniambia jibu."

Samsoni akamwambia, "Wala
sijamweleza baba yangu wala mama yangu,
kwa nini nikufumbulie?" 17 [e]Mkewe akalia
kwa muda wa zile siku zote saba za karamu.
Hivyo siku ile ya saba Samsoni akamweleza,
kwa kuwa aliendelea kumsisitiza sana. Naye
akawaeleza watu wake kile kitendawili.
18 Siku ya saba kabla ya jua kutua, watu
wa mji wakamwambia Samsoni,

"Ni nini kitamu kama asali?
Ni nini chenye nguvu kama
simba?"

Samsoni akawaambia,

"Kama hamkulima na mtamba
wangu,
hamngeweza kufumbua
kitendawili changu."

19 [f]Ndipo Roho wa Bwana akamjia
Samsoni kwa nguvu. Akateremka mpaka
Ashkeloni, akawaua watu waume thelathini
miongoni mwa watu wa mji, akatwaa
mali zao na nguo zao, akawapa watu wale
waliofumbua kile kitendawili. Akiwa na
hasira, akakwea kurudi nyumbani kwa
baba yake. 20 [g]Lakini huyo mke wa Samsoni
akakabidhiwa kwa rafiki yake Samsoni
ambaye alikuwa rafiki yake msaidizi siku
ya arusi.

### *Kisasi Cha Samsoni Kwa Wafilisti*

15 [h]Baada ya kitambo kidogo, wakati wa
mavuno ya ngano, Samsoni akachukua
mwana-mbuzi, kwenda kumzuru mkewe.
Akasema, "Nataka kuingia chumbani
kwa mke wangu." Lakini baba yake huyo
mwanamke hakumruhusu kuingia.
2 [i]Huyo baba mkwe wake akamwambia,
"Nilikuwa na hakika kwamba ulimkataa,
hivyo mimi nikampa rafiki yako. Je, mdogo

---

[a] **14:10** Mwa 29:2
[b] **14:12** Hes 12:8; Eze 17:2; 20:49; 24:3; Hos 12:10; Mwa 29:27; 45:22
[c] **14:15** Amu 16:5; Mhu 7:26; Law 20:14-16; Amu 15:6
[d] **14:16** Amu 16:15
[e] **14:17** Es 1:5
[f] **14:19** Amu 3:10; 2Nya 24:20; Yos 13:3; Isa 11:2; 1Sam 11:6
[g] **14:20** Amu 15:2, 6; Yn 3:29
[h] **15:1** Mwa 30:14; Amu 13:24; Mwa 38:17; 29:21
[i] **15:2** Amu 14:20

wake wa kike si mzuri zaidi kuliko yeye?
Mchukue huyo badala yake.”
[3] Samsoni akawaambia, “Wakati huu,
nitakapowadhuru Wafilisti, sitakuwa
na lawama.” [4] [a]Hivyo Samsoni akatoka
akawakamata mbweha 300 na kuwafunga
wawili wawili kwa mikia yao kila mmoja
kwa mwingine. Kisha akafungia mwenge
wa moto, kwenye mikia ya kila jozi
moja ya mbweha aliyokuwa ameifunga,
[5] [b]akawasha ile mienge na kuwaachia wale
mbweha katika mashamba ya Wafilisti ya
nafaka zilizosimamishwa katika matita.
Akateketeza matita ya nafaka zilizosimama,
pamoja na mashamba ya mizabibu na
viunga vya mizeituni.
[6] [c]Ndipo Wafilisti wakauliza, “Ni nani
aliyetenda jambo hili?” Wakaambiwa,
“Ni Samsoni, yule mkwewe Mtimna,
kwa sababu alimchukua mkewe akampa
mwenzake.”
Hivyo Wafilisti wakapanda
wakamteketeza kwa moto yeye huyo
mwanamke pamoja na baba yake. [7] Samsoni
akawaambia, “Kwa kuwa mmetenda hivyo,
hakika sitatulia mpaka niwe nimelipiza
kisasi juu yenu.” [8] [d]Akawashambulia kwa
ukali kwa mapigo makuu na kuwaua watu
wengi sana. Kisha akateremka na kukaa
katika ufa kwenye mwamba wa Etamu.
[9] Wafilisti wakapanda na kupiga kambi
huko Yuda na kuenea huko Lehi. [10] Watu
wa Yuda wakawauliza, “Kwa nini mmekuja
kupigana nasi?”
Wakawajibu, “Tumekuja ili kumkamata
Samsoni na kumtenda kama alivyotutendea.”
[11] [e]Ndipo watu 3,000 toka Yuda
walipoteremka na kwenda kwenye ufa
wa mwamba huko Etamu, na kumwambia
Samsoni, “Je, hujatambua kuwa Wafilisti
wanatutawala? Ni nini hiki ulichotutendea?”
Akawajibu, “Mimi nimewatendea tu kile
walichonitendea.”
[12] [f]Wakamwambia, “Tumekuja kukufunga
na kukutia mikononi mwa Wafilisti.”
Samsoni akawaambia, “Niapieni kuwa
hamtaniua ninyi wenyewe.”
[13] [g]Wakamjibu, “Sisi hatutakuua, bali
tutakufunga tu na kukutia mikononi
mwao.” Basi wakamfunga kwa kamba mbili
mpya. Wakamchukua toka huko kwenye
ufa katika mwamba. [14] [h]Alipokaribia Lehi,
Wafilisti wakamjia wakipiga kelele. Roho
wa BWANA akamjia juu yake kwa nguvu.
Kamba zilizomfunga mikono yake zikawa
kama kitani iliyochomwa kwa moto, na
vifungo vyake vikaanguka chini toka
mikononi mwake. [15] [i]Ndipo akaona mfupa
mpya wa taya la punda, akanyoosha mkono,
akauchukua na kuua nao Wafilisti wapatao
1,000.
[16] [j]Ndipo Samsoni akasema,

“Kwa taya la punda
  malundo juu ya malundo.
Kwa taya la punda
  nimeua watu 1,000.”

[17] Alipomaliza kusema, akautupa ule
mfupa wa taya; na mahali pale pakaitwa
Ramath-Lehi.[k]
[18] [l]Kwa kuwa alikuwa amesikia kiu sana,
akamlilia BWANA akisema, “Umempa
mtumishi wako ushindi huu mkuu. Je, sasa
nife kwa kiu na kuangukia mikononi mwa
hawa watu wasiotahiriwa?” [19] [m]BWANA
akafunua shimo huko Lehi, pakatoka maji.
Samsoni alipoyanywa, nguvu zikamrudia
na kuhuika. Hivyo chemchemi ile ikaitwa
En-Hakore,[n] nayo iko mpaka leo huko Lehi.
[20] [o]Samsoni akawa mwamuzi wa Waisraeli

---

[a]**15:4** Wim 2:15; Mwa 15:17
[b]**15:5** Mwa 15:17; Kut 22:6; 2Sam 14:30-31
[c]**15:6** Amu 14:20; Mwa 38:24; Amu 14:15
[d]**15:8** Isa 2:21
[e]**15:11** Amu 13:1; 14:4; Za 106:40-42
[f]**15:12** Mwa 47:31
[g]**15:13** Amu 16:11-12
[h]**15:14** Amu 3:10; Yos 2:6; Amu 14:19; 1Sam 11:6
[i]**15:15** Law 26:8; Yos 23:10
[j]**15:16** Yer 22:19
[k]17 Ramath-Lehi maana yake Kilima cha Taya.
[l]**15:18** Amu 16:28; Kum 20:4
[m]**15:19** Mwa 45:27; 1Sam 30:12; Isa 40:29; Kut 17:6
[n]19 En-Hakore maana yake ni Chemchemi ya Aliyeita.
[o]**15:20** Amu 13:1; 16:31; Ebr 11:32

katika siku za Wafilisti kwa muda wa miaka
ishirini.

*Samsoni Na Delila*

16 [a]Siku moja Samsoni alienda Gaza,
akamwona mwanamke kahaba,
naye akaingia kwake. 2 [b]Watu wa Gaza
wakaambiwa, “Samsoni amekuja huku!”
Hivyo wakapazingira mahali pale nao
wakamvizia usiku kucha, penye lango la
mji. Wakanyamaza kimya usiku kucha,
wakisema, “Tumvizie hadi mapambazuko,
ndipo tutamuua.”
3 [c]Samsoni akalala mpaka usiku wa
manane. Akaondoka katikati ya usiku,
akashika milango ya lango la mji pamoja
na miimo yake miwili, akaing’oa, makomeo
yake na vyote. Akaviweka mabegani mwake
na kuvipeleka mpaka kwenye kilele cha
mlima ule unaokabili Hebroni.
4 [d]Baada ya hayo akampenda
mwanamke mmoja katika Bonde la
Soreki aliyeitwa Delila. 5 [e]Viongozi wa
Wafilisti wakamwendea yule mwanamke
na kumwambia, “Umbembeleze ili upate
kujua siri za nguvu zake zilizo nyingi na
jinsi tutakavyoweza kumshinda ili tuweze
kumfunga na kumtiisha. Nasi kila mmoja
wetu tutakupa shekeli 1,100 za fedha.”[f]
6 Hivyo Delila akamwambia Samsoni,
“Naomba niambie siri ya hizi nguvu zako
nyingi na jinsi utakavyoweza kufungwa ili
kukutiisha.”
7 Samsoni akamjibu, “Kama wakinifunga
kwa kamba saba za upinde ambazo
hazijakauka bado, hapo ndipo nitakapokuwa
dhaifu kama mtu mwingine yeyote.”
8 Viongozi wa Wafilisti wakamletea
yule mwanamke kamba saba za upinde
ambazo hazijakauka bado, akamfunga
nazo Samsoni. 9 Wakati watu wakiwa
wanamvizia katika chumba cha ndani,
yule mwanamke akamwambia, “Samsoni,
Wafilisti wanakujia!” Lakini yeye akazikata
zile kamba za upinde, kama vile uzi wa
pamba unapoguswa na moto. Hivyo siri ya
nguvu zake haikujulikana.
10 Ndipo Delila akamwambia Samsoni,
“Umenifanyia mzaha na kuniambia uongo.
Tafadhali niambie waweza kufungwa kwa
kitu gani?”
11 [g]Akamwambia, “Wakinifunga kwa
uthabiti kwa kamba mpya ambazo
hazijatumika, basi nitakuwa dhaifu kama
mtu mwingine yeyote.”
12 Hivyo Delila akachukua kamba mpya
na kumfunga nazo. Kisha akamwambia,
“Samsoni, Wafilisti wanakujia!” Wale watu
waliokuwa wanamvizia walikuwa katika
chumba cha ndani. Lakini akazikata zile
kamba zilizokuwa zimefunga mikono yake
kama akatavyo uzi.
13 Ndipo Delila akamwambia Samsoni,
“Mpaka sasa, umenifanyia mzaha na
kuniambia uongo. Nieleze ni jinsi gani
utakavyoweza kufungwa.”
Samsoni akamwambia, “Kama ukivisuka
hivi vishungi saba vya nywele za kichwa
changu katika mtande wa nguo na kukaza
kwa msumari, ndipo nitakuwa dhaifu kama
mtu mwingine yeyote.” Hivyo Samsoni
alipokuwa amelala, Delila akachukua vile
vishungi saba vya nywele za kichwa chake
na kuvifunga kwenye mtande wa nguo,
14 na kuvikaza kwa msumari.
Kisha akamwambia, “Samsoni, Wafilisti
wanakujia!” Lakini akaamka kutoka
usingizini na kuung’oa ule msumari na
ule mtande.
15 [h]Ndipo Delila akamwambia, “Wawezaje
kusema, ‘Nakupenda,’ wakati moyo wako
haupo pamoja nami? Umenifanyia mzaha
mara hizi tatu na hujaniambia siri ya hizi
nguvu zako nyingi.” 16 Hatimaye, baada ya
kuwa anamsumbua kwa maneno siku kwa
siku na kumuudhi, roho yake ikataabika
hata kufa.
17 [i]Hivyo akamwambia yule mwanamke
siri yake yote, akamwambia, “Wembe
haujapita kamwe kichwani mwangu, kwa

[a]**16:1** Amu 16:28; Mwa 10:19; 38:15
[b]**16:2** Yos 2:5; 1Sam 19:11; Mdo 9:24
[c]**16:3** Yos 10:36
[d]**16:4** Mwa 24:67; 34:3
[e]**16:5** Yos 13:3; Kut 10:7; Amu 14:15
[f]5 Shekeli 1,100 za fedha ni sawa na kilo 13 za fedha.
[g]**16:11** Amu 15:13
[h]**16:15** Hes 24:10; Amu 14:16
[i]**16:17** Hes 6:2; 15:9; Amu 13:5

kuwa mimi ni Mnadhiri wa Mungu tangu tumboni mwa mama yangu. Kama nywele za kichwa changu zikinyolewa, nguvu zangu zitanitoka, na nitakuwa dhaifu kama mtu mwingine yeyote!”

18 [a]Delila alipoona kuwa amemweleza siri yake yote, akatuma ujumbe kwa viongozi wa Wafilisti na kusema, “Njooni tena mara nyingine, maana amenieleza siri yake yote.” Basi viongozi wa Wafilisti wakaja kwa Delila, wakiwa na fedha mikononi
mwao. 19 [b]Delila akamfanya alale usingizi magotini pake, akamwita mtu akamnyoa vile vishungi saba vya nywele za kichwa chake. Akaanza kumsumbua ili aamke nazo nguvu zake zikamtoka.

20 [c]Yule mwanamke akamwita, “Samsoni, hao Wafilisti wanakujia!”

Akaamka toka usingizini akasema, “Nitatoka nje kama hapo awali, nitawakung’utia mbali na kuwa huru.” Lakini hakujua kuwa Bwana amemwacha.

21 [d]Basi Wafilisti wakamkamata, wakamng’oa macho yake, wakamchukua wakamteremsha mpaka Gaza. Wakiwa wamemfunga kwa pingu za shaba, wakamweka ili asage ngano huko gerezani.
22 Wakati huo nywele za kichwa chake zikaanza kukua tena baada ya kunyolewa.

*Kifo Cha Samsoni*

23 [e]Basi viongozi wa Wafilisti wakakusanyika pamoja ili kutoa kafara kwa mungu wao Dagoni na kufanya karamu, wakisema, “Mungu wetu amemtia adui yetu Samsoni mikononi mwetu.”

24 [f]Watu walipomwona Samsoni wakamsifu mungu wao, wakisema:

“Sasa mungu wetu amemtia adui yetu
mikononi mwetu,
yule aliyeharibu nchi yetu
na kuwaua watu wengi miongoni mwetu.”

25 [g]Mioyo yao ilipokuwa imefurahishwa wakasema, “Mleteni Samsoni aje acheze ili tufurahi.” Basi wakamleta Samsoni kutoka mle gerezani naye akacheza mbele yao.

Wakamweka kati ya nguzo mbili.
26 Samsoni akamwambia mtumishi aliyeshika mkono wake, “Niweke mahali ambapo ninaweza kuzigusa nguzo ambazo zinategemeza jengo ili nipate kuziegemea.”
27 [h]Basi lile jengo lilikuwa na wingi wa watu waume kwa wake; viongozi wote wa Wafilisti walikuwamo humo, na kwenye sakafu ya juu walikuwepo watu 3,000 waume kwa wake, waliokuwa wakimtazama
Samsoni wakati anacheza. 28 [i]Ndipo
Samsoni akamwomba Bwana, akasema, “Ee Bwana Mwenyezi, unikumbuke. Ee Mungu, nakusihi ukanitie nguvu mara hii moja tena, ili kwa tendo hili nipate kulipiza kisasi juu ya Wafilisti kwa ajili ya
macho yangu mawili.” 29 Ndipo Samsoni
akazikaribia zile nguzo mbili za katikati ambazo lile jengo lilikuwa linazitegemea. Akazishika moja kwa mkono wa kuume na
nyingine mkono wa kushoto. 30 Samsoni
akasema, “Nife pamoja na Wafilisti!” Ndipo akazisukuma zile nguzo kwa nguvu zake zote, lile jengo likaanguka juu ya viongozi na watu wote waliokuwamo mle ndani yake. Hivyo akawaua watu wengi wakati wa kufa kwake kuliko siku za uhai wake.

31 [j]Basi ndugu zake na jamaa yote ya baba yake wakateremka kwenda kumchukua. Wakampandisha na kumzika kati ya Sora na Eshtaoli kwenye kaburi la Manoa baba yake. Naye Samsoni alikuwa mwamuzi wa Israeli kwa miaka ishirini.

*Sanamu Za Mika*

17 [k]Palikuwa na mtu aliyeitwa Mika ambaye aliishi katika vilima vya

[a]**16:18** Yos 13:3; 1Sam 5:8
[b]**16:19** Mit 7:26-27
[c]**16:20** Hes 14:42; Yos 7:12; 1Sam 16:14; 18:12; 28:15
[d]**16:21** Yer 47:1; Hes 16:14; Mwa 10:19; Ay 31:10; Isa 47:2
[e]**16:23** 1Sam 5:3; 1Nya 10:10
[f]**16:24** Dan 5:4; 1Sam 31:9; 1Nya 10:9
[g]**16:25** Amu 9:27; 19:6-9, 22; Rut 3:7; Es 1:10
[h]**16:27** Yos 2:8; Kum 22:8
[i]**16:28** Yos 15:18; Yer 15:15
[j]**16:31** Amu 13:2; Rut 1:1; 1Sam 7:6; Amu 15:20
[k]**17:1** Amu 18:2, 13

Efraimu. 2 [a]Akamwambia mama yake, “Zile
shekeli 1,100[b] za fedha zilizochukuliwa
kwako, ambazo nilisikia ukizinenea
maneno ya laana, hizi hapa; mimi ndiye
niliyezichukua, lakini sasa ninakurudishia.”

Ndipo mama yake akamwambia, “BWANA
na akubariki, mwanangu.”

3 [c]Alipozirudisha zile shekeli 1,100
za fedha kwa mama yake, mama yake
akamwambia, “Mimi nimeiweka fedha hii
wakfu kwa BWANA kwa ajili ya mwanangu
kutengenezea kinyago cha kuchonga na
sanamu ya kusubu. Mimi nitakurudishia
wewe.”

4 [d]Hivyo akamrudishia mama yake
ile fedha, naye mama yake akachukua
shekeli mia mbili[e] za hiyo fedha na kumpa
mfua fedha, ambaye aliifanyiza kinyago
na sanamu. Navyo vikawekwa ndani ya
nyumba ya Mika.

5 [f]Basi Mika alikuwa na mahali pa
kuabudia miungu, akatengeneza naivera,
pamoja na vinyago, na kumweka mmoja
wa wanawe kuwa kuhani wake. 6 [g]Katika
siku hizo Israeli hawakuwa na mfalme, kila
mmoja akafanya kama alivyoona vyema
machoni pake mwenyewe.

7 [h]Basi palikuwa na kijana mmoja
wa Bethlehemu ya Yuda. Yeye alikuwa
Mlawi aliyeishi miongoni mwa kabila la
Yuda. 8 Huyu kijana akatoka katika mji
huo wa Bethlehemu ya Yuda na kutafuta
mahali pengine ambapo angeweza kuishi.
Alipokuwa akisafiri, akafika nyumbani kwa
Mika katika vilima vya Efraimu.

9 Mika akamuuliza, “Wewe umetoka
wapi?”

Akamjibu, “Mimi ni Mlawi kutoka
Bethlehemu ya Yuda, ninatafuta mahali
pa kuishi.”

10 [i]Ndipo Mika akamwambia, “Ishi pamoja
nami, uwe baba yangu na kuhani wangu,
nami nitakupa shekeli kumi[j] za fedha, nguo
na chakula.” 11 Hivyo yule Mlawi akakubali
kuishi pamoja naye, naye huyo kijana akawa
kwake kama mmoja wa wanawe. 12 [k]Hivyo
Mika akamweka wakfu huyo kijana Mlawi,
naye huyo akawa kuhani wake na kuishi
nyumbani mwake. 13 [l]Ndipo Mika akasema,
“Sasa najua BWANA atanitendea mema,
kwa kuwa Mlawi huyu amekuwa kuhani
wangu.”

### *Wadani Wahamia Laishi*

18 [m]Katika siku hizo Israeli walikuwa
hawana mfalme.

Katika siku hizo kabila la Wadani
walikuwa wanatafuta mahali pao wenyewe
pa kuishi, kwa sababu walikuwa hawajafika
kwenye urithi wao miongoni mwa makabila
ya Israeli. 2 [n]Hivyo Wadani wakatuma
mashujaa watano kutoka Sora na Eshtaoli
ili kupeleleza nchi na kuichunguza.
Hawa watu waliwakilisha koo zao zote.
Waliwaambia, “Nendeni mkaichunguze
hiyo nchi.”

Watu hao wakaingia katika nchi ya vilima
ya Efraimu, nao wakafika nyumba ya Mika,
ambako walilala usiku huo. 3 [o]Walipofika
karibu na nyumba ya Mika, waliitambua
sauti ya yule kijana Mlawi; hivyo wakaingia
humo na kumuuliza, “Ni nani aliyekuleta
hapa? Unafanya nini mahali hapa? Kwa
nini uko hapa?”

4 [p]Akawaeleza yale Mika aliyomtendea,
naye akasema, “Ameniajiri nami ni kuhani
wake.”

---

[a]**17:2** Rut 2:20; 3:10; 1Sam 15:13; 23:21; 2Sam 2:5
[b]2 Shekeli 1,100 za fedha ni sawa na kilo 13 za fedha.
[c]**17:3** Kut 34:17; Law 19:4; Kut 20:4
[d]**17:4** Kut 32:4; Isa 17:8
[e]4 Shekeli 200 za fedha ni sawa na kilo 2.3 za fedha.
[f]**17:5** Isa 44:13; Eze 8:10; Amu 8:27; Mwa 31:19; Hes 16:10; Kut 29:9; Amu 18:24
[g]**17:6** Amu 18:1; 19:1; 21:25; Kum 12:8
[h]**17:7** Amu 18:3; Mwa 35:19; Mik 5:2; Mt 2:1
[i]**17:10** Mwa 45:8; Amu 18:19
[j]10 Shekeli 10 za fedha ni sawa na gramu 115 za fedha.
[k]**17:12** Hes 16:10; Amu 18:4
[l]**17:13** Hes 18:7
[m]**18:1** Amu 17:6; Yos 19:47; Amu 1:34
[n]**18:2** Mwa 30:6; Hes 21:32; Yos 2:1; Amu 17:1
[o]**18:3** Amu 17:7
[p]**18:4** Amu 17:12

5 [a]Kisha wakamwambia, “Tafadhali
tuulizie kwa Mungu kama safari yetu
itafanikiwa.”
6 [b]Yule kuhani akawajibu, “Enendeni kwa
amani. Safari yenu ina kibali cha BWANA.”
7 [c]Basi hao watu watano wakaondoka na
kufika Laishi, mahali ambapo waliwakuta
watu wanaishi salama, kama Wasidoni,
kwa utulivu na bila mashaka. Nchi yao
haikupungukiwa na kitu chochote, hivyo
wakawa tajiri. Pia walikaa mbali sana na
Wasidoni, wala hawakushughulika na mtu
yeyote.
8 Waliporudi kwa ndugu zao huko Sora
na Eshtaoli, ndugu zao wakawauliza,
“Mlionaje mambo huko?”
9 [d]Wakajibu, “Twendeni, tukapigane
nao! Tumeona kuwa nchi ni nzuri sana.
Je, hamtafanya chochote? Msisite kupanda
ili kuimiliki. 10 [e]Mtakapokwenda huko
mtakuta watu waliotulia walio salama,
nayo nchi hiyo ni kubwa na Mungu ameitia
mikononi mwenu, nayo ni nchi ambayo
haikupungukiwa na kitu chochote kilicho
duniani.”
11 [f]Ndipo watu 600 toka ukoo wa Wadani,
waliojifunga silaha za vita, wakaondoka
Sora na Eshtaoli. 12 [g]Walipokuwa wakisafiri
wakapiga kambi huko Kiriath-Yearimu
katika Yuda. Hii ndiyo sababu sehemu
ya magharibi ya Kiriath-Yearimu inaitwa
Mahane-Dani[h] mpaka leo. 13 [i]Kutoka hapo
wakaendelea mbele mpaka nchi ya vilima
ya Efraimu na kufika katika nyumba ya
Mika.
14 [j]Ndipo wale watu watano waliopeleleza
nchi ya Laishi wakawaambia ndugu zao,
“Je, mwajua kuwa mojawapo ya nyumba
hizi kuna naivera, sanamu ndogo za
nyumbani, sanamu ya kuchonga na sanamu
ya kusubu? Sasa basi fikirini mtakalofanya.”
15 Basi wakaingia humo na kwenda kwenye
nyumba ya yule kijana Mlawi katika
nyumba ya Mika na kumsalimu. 16 Wale
Wadani 600, waliovaa silaha za vita,
wakasimama penye ingilio la lango. 17 [k]Wale
watu watano waliokwenda kupeleleza nchi
wakaingia ndani na kuchukua ile sanamu
ya kuchonga, ile naivera, na zile sanamu
nyingine ndogo za nyumbani pamoja na
ile sanamu ya kusubu, wakati yule kuhani
akiwa amesimama pale penye ingilio la
lango pamoja na wale watu 600 waliokuwa
wamejifunga silaha za vita.
18 [l]Hao watu walipoingia katika nyumba
ya Mika na kuchukua ile sanamu ya
kuchonga, ile naivera, na zile sanamu
nyingine ndogo za nyumbani, pamoja na ile
sanamu ya kusubu, yule kuhani akawauliza,
“Mnafanya nini?”
19 [m]Wakamjibu, “Nyamaza kimya! Weka
mkono wako juu ya kinywa chako na
ufuatane nasi, uwe baba yetu na kuhani
wetu. Si ni afadhali utumikie kabila
na ukoo katika Israeli kama kuhani
kuliko kumtumikia mtu mmoja na watu
wa nyumbani mwake?” 20 Yule kuhani
akafurahi. Akachukua ile naivera, zile
sanamu nyingine ndogo za nyumbani, na
sanamu ya kuchonga, naye akaenda pamoja
na wale watu. 21 Ndipo wakageuka na
kuondoka wakiwatanguliza mbele watoto
wao wadogo, wanyama wao wa kufugwa
na mali zao.
22 Walipokuwa wamesafiri umbali kidogo
toka nyumbani kwa Mika, watu walioishi
karibu na Mika wakaitwa wakakusanyika
pamoja, nao wakawafikia Wadani.
23 Walipofuatilia wakipiga kelele Wadani
wakawageukia na kumwambia Mika, “Una
nini wewe hata ukaja na kundi la watu
namna hii ili kupigana?”
24 Akawajibu, “Mmechukua miungu yote
niliyoitengeneza, mkachukua na kuhani

[a]**18:5** Mwa 25:22; Amu 20:18, 23, 27; 1Sam 14:18; 2Sam 5:19; 2Fal 1:2; 8:8
[b]**18:6** 1Fal 22:6
[c]**18:7** Yos 19:47; Mwa 34:25; Yos 11:8
[d]**18:9** Hes 13:30; 1Fal 22:3
[e]**18:10** Kum 8:9; 1Nya 4:40
[f]**18:11** Amu 13:2
[g]**18:12** Yos 9:17; Amu 13:25
[h]12 Mahane-Dani maana yake Kambi ya Dani.
[i]**18:13** Amu 17:6
[j]**18:14** Yos 19:47; Amu 8:27; Mwa 31:19; Amu 17:5
[k]**18:17** Mwa 31:19; Mik 5:13
[l]**18:18** Isa 46:2; Yer 43:11; 48:7; 49:3; Hos 10:5; Mwa 31:19
[m]**18:19** Ay 13:5; 21:5; 29:9; 40:4; Isa 52:15; Mik 7:16; Amu 17:10; Hes 26:42

wangu, nanyi mkaondoka. Nimebaki na
nini kingine? Mnawezaje kuniuliza, 'Una
nini wewe?' "
25 Wadani wakamjibu, "Usibishane
na sisi, la sivyo watu wenye hasira kali
watakushambulia, nawe na watu wa
nyumbani mwako mtapoteza maisha."
26 [a]Basi Wadani wakaenda zao, naye Mika
alipoona kuwa wana nguvu kumliko yeye,
akageuka na kurudi nyumbani kwake.
27 [b]Kisha wakachukua vile Mika
alivyokuwa ametengeneza, na kuhani
wake, wakaendelea hadi Laishi, dhidi
ya watu walio na amani, wasiokuwa na
wasiwasi. Wakawashambulia kwa upanga
na kuuteketeza mji wao kwa moto.
28 Hapakuwa na yeyote wa kuwaokoa, kwa
kuwa kulikuwa mbali sana na Sidoni na
hawakuwa na ushirikiano na mtu mwingine
yeyote. Mji ulikuwa kwenye bonde karibu
na Beth-Rehobu.
Wadani wakaujenga upya huo mji na
kuishi humo. 29 Wakauita ule mji Dani
kwa kufuata jina la baba yao aliyezaliwa
na Israeli, ingawa mji huo ulikuwa
ukiitwa Laishi hapo kwanza. 30 [c]Kisha
Wadani wakajisimamishia sanamu ile ya
kuchonga, naye Yonathani mwana wa
Gershomu, mwana wa Mose pamoja na
wanawe walikuwa makuhani wa kabila
la Wadani mpaka nchi hiyo ilipotekwa.
31 [d]Wakaisimamisha na kuiabudu hiyo
sanamu ya kuchonga ya Mika aliyokuwa
ameitengeneza, wakati wote ule nyumba
ya Mungu ilipokuwa huko Shilo.

*Mlawi Na Suria Wake*

19 [e]Katika siku hizo Israeli hawakuwa na
mfalme.
Basi Mlawi mmoja aliyeishi sehemu za
mbali katika nchi ya vilima ya Efraimu,
akamchukua suria mmoja kutoka
Bethlehemu ya Yuda. 2 Lakini suria wake
akafanya ukahaba dhidi yake, naye
akamwacha akarudi nyumbani kwa baba
yake huko Bethlehemu ya Yuda. Baada ya
kukaa huko kwa muda wa miezi minne,
3 mume wake akaenda kumsihi ili arudi.
Alikwenda na mtumishi wake na punda
wawili. Yule mwanamke akamkaribisha
nyumbani mwa baba yake, baba yake
alipomwona akamkaribisha kwa furaha.
4 [f]Baba mkwe wake, yaani, baba yake yule
msichana, akamzuia ili akae, hivyo akakaa
na huyo baba mkwe wake kwa siku tatu,
wakila, wakinywa na kulala huko.
5 [g]Siku ya nne wakaamka mapema naye
akajiandaa kuondoka, lakini baba wa
yule msichana akamwambia mkwewe,
"Ujiburudishe kwa kula kitu chochote,
ndipo uweze kwenda." 6 [h]Basi wakaketi wote
wawili ili kula na kunywa pamoja. Baadaye
baba wa msichana akamwambia, "Tafadhali
ubakie usiku huu upate kujifurahisha nafsi
yako." 7 Basi yule mtu alipotaka kuondoka
baba wa yule msichana akamsihi, basi
akabaki usiku ule. 8 Asubuhi ya siku ya
tano, alipoamka ili aondoke, baba wa yule
msichana akamwambia, "Jiburudishe nafsi
yako. Ngoja mpaka mchana!" Kwa hiyo
wote wawili wakala chakula pamoja.
9 Basi wakati yule mtu alipoinuka aende
zake, pamoja na suria wake na mtumishi
wake, baba mkwe wake, yaani, baba wa
yule msichana akamwambia, "Tazama
sasa jioni inakaribia. Ulale hapa usiku
unakaribia. Ukae, ukajifurahishe nafsi yako.
Kesho unaweza kuamka mapema asubuhi
na uende nyumbani kwako." 10 [i]Lakini
akakataa kulala tena, akaondoka na kwenda
mpaka Yebusi (ndio Yerusalemu), akiwa
na punda wake wawili waliotandikiwa,
pamoja na suria wake.
11 [j]Alipokaribia Yebusi na usiku ukiwa
umekaribia, mtumishi akamwambia bwana
wake, "Haya sasa natuingie katika mji huu
wa Wayebusi tulale humo."
12 Lakini bwana wake akamjibu, "Hapana.
Hatutaingia kwenye mji wa kigeni, ambao

[a]**18:26** 2Sam 3:39; Za 18:17; 35:10
[b]**18:27** Mwa 34:25; Hes 31:10; Mwa 49:17; Yos 19:47
[c]**18:30** Kut 2:22; Amu 17:3-5
[d]**18:31** Amu 19:18; 20:18; Yos 18:1; Yer 7:14
[e]**19:1** Amu 18:1; Rut 1:1
[f]**19:4** Kut 32:6
[g]**19:5** Mwa 15:8
[h]**19:6** Amu 16:25
[i]**19:10** Mwa 10:16; Yos 15:8; 1Nya 11:4-5
[j]**19:11** Mwa 10:16; Yos 3:10

watu wake si Waisraeli. Tutaendelea mpaka
tufike Gibea." 13 [a]Akasema, "Haya, tujitahidi
tufike Gibea au Rama, nasi tutalala katika
mji mmojawapo." 14 [b]Hivyo wakaendelea na
safari, jua likachwea walipokaribia Gibea
ambao ni mji wa Benyamini. 15 [c]Wakageuka
ili kuingia na kulala Gibea. Wakaingia
humo, wakaketi kwenye uwanja wa mji,
wala hakuna mtu yeyote aliyewakaribisha
kwake ili wapate kulala.

16 [d]Jioni ile mtu mmoja mzee toka nchi
ya vilima ya Efraimu, aliyekuwa anaishi
huko Gibea (watu wa sehemu ile walikuwa
Wabenyamini), akarudi kutoka kwenye kazi
za shamba. 17 [e]Alipotazama na kuwaona hao
wasafiri katika uwanja wa mji, yule mzee
akawauliza, "Ninyi mnakwenda wapi?
Nanyi mmetoka wapi?"

18 [f]Akamwambia, "Tumepita kutoka
Bethlehemu ya Yuda, tunaelekea katika
nchi ya vilima ya Efraimu, ambako ndiko
ninakoishi. Nilikwenda Bethlehemu ya
Yuda na sasa ninakwenda katika nyumba ya
BWANA. Hakuna mtu yeyote aliyenikaribisha
katika nyumba yake. 19 [g]Tunazo nyasi na
chakula cha punda wetu na mkate na
divai kwa ajili yetu sisi watumishi wako,
yaani mimi, mtumishi wako mwanamke,
pamoja na huyu kijana tuliyefuatana naye.
Hatuhitaji kitu chochote."

20 Yule mzee akawaambia, "Amani iwe
kwenu! Karibuni nyumbani mwangu.
Nitawapa mahitaji yenu yote, msilale katika
uwanja huu wa mji." 21 [h]Hivyo akamwingiza
nyumbani mwake na kuwalisha punda
wake. Baada ya kunawa miguu yao, wakala
na kunywa.

22 [i]Walipokuwa wakijiburudisha, watu
waovu wa mji huo, wakaizingira ile
nyumba. Wakagonga mlango na kusema na
yule mzee mwenye nyumba, "Mtoe nje yule
mtu aliyeingia kwako, tupate kumlawiti."

23 [j]Yule mwenye nyumba akatoka nje na
kuwaambia, "Hapana, ndugu zangu msiwe
waovu namna hii, ninawasihi. Kwa kuwa
huyu mtu ni mgeni wangu msifanye jambo
hili la aibu. 24 [k]Tazameni, hapa yupo binti
yangu ambaye ni bikira na suria wa huyu
mtu. Nitawatoleeni hawa sasa, mkawatwae
kwa nguvu na kuwafanyia lolote mtakalo.
Lakini kwa mtu huyu msimfanyie jambo
ovu hivyo."

25 [l]Lakini wale watu hawakumsikia.
Hivyo yule mtu akamtoa yule suria wake
nje kwa wale watu, nao wakambaka na
kumnajisi usiku ule kucha mpaka asubuhi.
Kulipoanza kupambazuka wakamwachia
aende. 26 Alfajiri yule mwanamke akarudi
kwenye ile nyumba bwana wake alikokuwa,
akaanguka chini mlangoni, akalala pale
hata kulipopambazuka.

27 Bwana wake alipoamka asubuhi na
kufungua mlango wa nyumba na kutoka nje
ili kuendelea na safari yake, tazama, yule
suria wake alikuwa ameanguka pale penye
ingilio la nyumba na mikono yake ikiwa
penye kizingiti cha chini. 28 Akamwambia
yule suria, "Inuka, twende." Lakini hakujibu.
Yule bwana akamwinua akampandisha
juu ya punda wake, wakaondoka kwenda
nyumbani.

29 [m]Alipofika nyumbani, akachukua kisu
na kumkatakata yule suria kiungo kwa
kiungo, sehemu kumi na mbili, na kuvipeleka
hivyo vipande katika sehemu zote za Israeli.
30 [n]Kila mtu aliyeona akasema, "Jambo la
namna hii halijaonekana wala kutendeka,
tangu Israeli walipopanda kutoka Misri.
Fikirini juu ya jambo hili! Tafakarini juu
ya jambo hili! Tuambieni tufanye nini!"

---

[a]**19:13** Yos 18:25
[b]**19:14** Yos 15:57; 1Sam 10:26; 11:4; 13:2; 15:34; Isa 10:29
[c]**19:15** Mwa 24:23; 19:2
[d]**19:16** Za 104:23
[e]**19:17** Mwa 29:4
[f]**19:18** Amu 18:31
[g]**19:19** Mwa 24:25; 42:27; 14:18
[h]**19:21** Mwa 24:32-33; Lk 7:44
[i]**19:22** Amu 16:25; Kum 13:13; Mwa 19:4-5; Amu 20:5; Rum 1:26-27
[j]**19:23** Mwa 19:6; 34:7; Law 19:29; Yos 7:15; Amu 20:6; Rum 1:27
[k]**19:24** Mwa 19:8; Kum 21:14
[l]**19:25** Mwa 20:5; 1Sam 31:4
[m]**19:29** Mwa 22:6; Amu 20:6; 1Sam 11:7
[n]**19:30** Hes 9:9; Amu 20:7; Mit 13:10

### *Waisraeli Wapigana Na Wabenyamini*

20 [a]Ndipo Waisraeli wote kuanzia Dani
hadi Beer-Sheba na wa kutoka nchi
ya Gileadi wakatoka kama mtu mmoja
wakakusanyika mbele za BWANA huko
Mispa. 2 [b]Viongozi wote wa kabila za
Israeli wakakaa kwenye nafasi zao katika
kusanyiko la watu wa Mungu, askari
400,000 waendao kwa miguu wenye
panga. 3 (Wabenyamini wakasikia kuwa
Waisraeli wamepanda kwenda Mispa.)
Ndipo Waisraeli wakasema, "Tuelezeni jinsi
jambo hili ovu lilivyotendeka."
4 [c]Hivyo yule Mlawi, mume wa yule
mwanamke aliyeuawa, akasema, "Mimi na
suria wangu tulifika Gibea ya Benyamini
ili tulale huko. 5 Wakati wa usiku watu wa
Gibea wakanijia na kuizingira nyumba,
wakitaka kuniua. Wakambaka suria wangu
mpaka akafa. 6 [d]Ndipo nikamchukua suria
wangu, nikamkatakata vipande vipande na
kuvipeleka katika nchi yote ya urithi wa
Israeli, kwa kuwa wametenda uasherati
mkubwa na jambo la aibu katika Israeli.
7 [e]Sasa, ninyi Waisraeli wote, semeni na
mtoe uamuzi wenu."
8 Watu wote wakainuka wakasema,
kama mtu mmoja, "Hakuna hata mmoja
wetu atakayekwenda nyumbani. Wala
hakuna hata mmoja wetu atakayerudi
nyumbani kwake. 9 [f]Sasa hili ndilo
tutakaloitendea Gibea: Tutaikabili jinsi
kura itakavyotuongoza. 10 Tutatoa watu
kumi katika kila 100 kutoka kwenye
kabila zote za Israeli, watu 100 katika
watu 1,000 na watu 1,000 katika 10,000,
ili waende wakalete mahitaji kwa ajili
ya jeshi. Basi wakati jeshi litakapofika
Gibea ya Benyamini, watawatendea yale
wanayostahili, kwa ajili ya uovu huu wa
aibu waliotenda katika Israeli." 11 Hivyo
wanaume wote wa Israeli wakakutanika
pamoja na kujiunga kama mtu mmoja dhidi
ya huo mji.
12 [g]Makabila ya Israeli yakatuma watu
kwenda katika kabila la Benyamini lote na
kuwaambia, "Ni uovu gani huu wa kutisha
uliotendeka katikati yenu? 13 [h]Basi watoeni
hao watu waovu kabisa walioko Gibea, ili
tupate kuwaua na kuondoa uovu katika
Israeli."
Lakini Wabenyamini hawakuwasikia
ndugu zao, Waisraeli. 14 Wakatoka katika
miji yao, wakakutanika Gibea ili kupigana
na Waisraeli. 15 Siku ile Wabenyamini
wakakusanya watu 26,000 kutoka miji
yao, waliojifunga panga, mbali na hao
700 waliochaguliwa miongoni mwa hao
waliokaa Gibea. 16 [i]Miongoni mwa hao
askari wote kulikuwa na watu 700 bora
waliochaguliwa watumiao mkono wa
kushoto, kila mmoja wao aliweza kutupa
jiwe kwa kombeo na kulenga unywele
mmoja bila kukosa.
17 Nao watu wa Israeli, mbali na hao wa
Benyamini, wakakusanya watu waume
400,000, wenye kutumia panga, wote hao
walikuwa mashujaa.
18 [j]Waisraeli wakapanda Betheli na
kumuuliza Mungu, "Ni nani miongoni
mwetu atakayetangulia mbele yetu ili
kupigana na Wabenyamini?"
BWANA akawajibu, "Yuda ndiye
atakayetangulia."
19 Asubuhi yake Waisraeli wakaamka na
kupiga kambi karibu na Gibea. 20 Waisraeli
wakatoka kupigana na Wabenyamini,
nao Waisraeli wakajiweka kwenye nafasi
zao katika vita dhidi yao huko Gibea.
21 Wabenyamini wakatoka Gibea na kuwaua
watu 22,000 wa Israeli siku ile. 22 Lakini
Waisraeli wakatiana moyo kila mmoja
na mwenzake, nao wakajiweka kwenye
nafasi zao katika vile vita mara ya pili
mahali pale walipokuwa wamejiweka
mara ya kwanza. 23 [k]Waisraeli wakapanda

---

[a]**20:1** Amu 21:5; Mwa 21:14; 1Sam 3:20; 2Sam 17:11; 24:15; 1Fal 4:25; 1Sam 11:7; 7:5; Yos 11:3
[b]**20:2** 1Sam 11:8; Amu 8:10
[c]**20:4** Yos 15:57; Mwa 24:23; Amu 19:15
[d]**20:6** Amu 19:29; 19:23; 2Sam 13:12; Yos 7:15
[e]**20:7** Amu 19:30
[f]**20:9** Law 16:8
[g]**20:12** Kum 13:13-14
[h]**20:13** Kum 13:13; 1Kor 5:13; Kum 13:5
[i]**20:16** Amu 3:15
[j]**20:18** Yos 12:9; Amu 18:31; 18:5; Mwa 49:10
[k]**20:23** Hes 14:1; Yos 7:6; Amu 18:5

mbele za BWANA na kulia mbele zake
mpaka jioni, nao wakamuuliza BWANA
wakisema, "Je, tupande tena kupigana vita
na Wabenyamini, ndugu zetu?"

BWANA akajibu, "Pandeni mkapigane
nao."

24 Ndipo Waisraeli wakawakaribia
Wabenyamini siku ya pili. 25 Wakati
huu, Wabenyamini walipotoka Gibea ili
kupigana nao, wakawaua watu Waisraeli
18,000, wote wakiwa wamejifunga panga.

26 [a]Ndipo Waisraeli, watu wote, wakapanda
Betheli, huko wakakaa mbele za BWANA
wakilia. Wakafunga siku ile mpaka jioni
na kutoa sadaka ya kuteketezwa na sadaka
ya amani kwa BWANA. 27 [b]Nao Waisraeli
wakauliza kwa BWANA. (Katika siku hizo
Sanduku la Agano la Mungu lilikuwa
huko 28 [c]na Finehasi mwana wa Eleazari,
mwana wa Aroni, alikuwa anahudumu
mbele za hilo Sanduku.) Wakauliza, "Je,
tupande kwenda vitani kupigana tena na
Wabenyamini ndugu zetu, au la?"

BWANA akajibu, "Nendeni, kwa kuwa
kesho nitawatia mikononi mwenu."

29 [d]Basi Waisraeli wakaweka waviziao
kuizunguka Gibea. 30 Kisha Waisraeli
wakapanda kupigana na Wabenyamini
katika siku ya tatu na kujiweka
kwenye nafasi zao dhidi ya Gibea kama
walivyokuwa wamefanya hapo kwanza.
31 [e]Wabenyamini wakatoka ili kukabiliana
nao, Waisraeli wakawavuta Wabenyamini
watoke katika mji. Wakaanza kupigana na
kuua watu wapatao thelathini wa Israeli,
kama walivyofanya nyakati nyingine,
katika njia kuu, moja iendayo Betheli na
nyingine Gibea.

32 Wabenyamini wakafikiri, "Wanapigwa
mbele yetu kama hapo kwanza." Waisraeli
wakasema, "Sisi na turudi nyuma ili
tuwavute wauache mji waende kuelekea
barabarani."

33 [f]Watu wote wa Israeli wakaondoka
kwenye sehemu zao na kujipanga huko Baal-
Tamari, nao wale waviziaji wa Waisraeli,
wakatoka hapo walipokuwa kwenye
uwanda wa magharibi ya Gibea. 34 [g]Ndipo
watu 10,000 bora waliochaguliwa katika
Israeli wote, wakaja kuishambulia Gibea.
Vita vilikuwa vikali sana, hata Wabenyamini
hawakutambua kuwa maangamizi yalikuwa
karibu nao kwa kiasi hicho. 35 [h]BWANA
akawashinda Wabenyamini mbele ya
Waisraeli na siku ile Waisraeli wakawaua
Wabenyamini watu waume 25,100, wote
wakiwa wenye kujifunga silaha za vita.
36 [i]Hivyo Wabenyamini wakaona kuwa
wamepigwa.

Basi Waisraeli walikuwa wameondoka
mbele ya Wabenyamini, kwa sababu
Waisraeli waliwategemea hao waviziaji
waliokuwa wamewaweka dhidi ya Gibea.
37 [j]Wale waviziaji wakafanya haraka kuingia
Gibea, wakasambaa na kuwaua watu
wote wa mji kwa upanga. 38 [k]Waisraeli
walikuwa wamepatana na hao waviziaji
kuwa wangefanya lipande wingu kubwa la
moshi kutoka huo mji, 39 [l]ndipo watu wa
Waisraeli wangegeuka kupigana.

Watu wa Benyamini walikuwa wameanza
kuwapiga na kuua watu wa Israeli (wapatao
thelathini), hivyo wakafikiri, "Hakika
tutawapiga, kama tulivyowashinda katika
vita hapo kwanza." 40 [m]Lakini wakati lile
wingu la moshi lilipoanza kupanda kutoka
ule mji, Wabenyamini wakageuka na kuona
moshi wa mji mzima unapaa juu angani.
41 [n]Ndipo watu wa Israeli wakawageukia,
nao Wabenyamini wakatiwa hofu,
kwa kuwa walitambua kwamba maafa
yamewajia. 42 Basi wakakimbia mbele
ya Waisraeli kuelekea nyikani, lakini
hawakuweza kukwepa vile vita. Nao

---

[a]**20:26** Hes 14:1; 2Sam 12:21; Kut 32:6; Amu 21:4; Law 1:3
[b]**20:27** Amu 18:5; Hes 10:33
[c]**20:28** Hes 25:7; Kum 18:5; Yos 2:24; 24:33; Amu 7:9
[d]**20:29** Yos 8:2-4
[e]**20:31** Yos 8:16; 16:1
[f]**20:33** Yos 8:19
[g]**20:34** Yos 8:14; Isa 47:11
[h]**20:35** 1Sam 9:21
[i]**20:36** Yos 8:15
[j]**20:37** Yos 8:19
[k]**20:38** Yos 8:20; 8:4-8
[l]**20:39** Za 78:9
[m]**20:40** Yos 8:20
[n]**20:41** Yos 8:21

watu wa Israeli waliotoka katika ile
miji wakawaua huko. 43 Wakawazingira
Wabenyamini pande zote, wakawafuatia
na kuwapata hapo walipopumzika katika
viunga vya Gibea upande wa mashariki.
44 [a]Wakaanguka Wabenyamini 18,000
ambao wote ni mashujaa. 45 [b]Walipogeuka
na kukimbia kuelekea nyikani hata kufikia
mwamba wa Rimoni, Waisraeli wakawaua
watu 5,000 wakiwa njiani. Wakawafuata
kwa kasi mpaka Gidomu huko wakawaua
watu wengine 2,000.

46 [c]Siku ile wakawaua Wabenyamini
25,000 waliokuwa mashujaa wa vita.
47 Lakini watu 600 wakakimbia kuelekea
nyikani katika mwamba wa Rimoni,
na kukaa huko muda wa miezi minne.
48 [d]Waisraeli wakarudi na kuua watu wote
wa Benyamini, pamoja na wanyama na
kila walichokikuta. Pia kila mji waliouona
waliuchoma moto.

*Wabenyamini Watafutiwa Wake*

21 [e]Wana wa Israeli walikuwa wameapa
kwa kiapo kule Mispa: "Hapana mtu
yeyote atakayemwoza binti yake kwa
Wabenyamini."

2 Watu wakaenda Betheli, wakaketi
mbele za Mungu mpaka jioni, wakapaza
sauti zao, wakalia sana. 3 Wakasema, "Ee
BWANA, Mungu wa Israeli, kwa nini jambo
hili limewapata Waisraeli? Kwa nini kabila
moja la Israeli limekosekana?"

4 [f]Kesho yake asubuhi na mapema watu
wakajenga madhabahu na kuleta sadaka za
kuteketezwa na sadaka za amani.

5 [g]Ndipo Waisraeli wakasema, "Ni kabila
lipi la Israeli ambalo halikufika katika
mkutano kumkaribia BWANA?" Kwa kuwa
walikuwa wameweka kiapo kikuu kuwa
yeyote asiyefika mbele za BWANA huko
Mispa, kwa hakika angeuawa.

6 Basi Waisraeli wakaghairi kwa ajili
ya ndugu zao Wabenyamini, wakasema,
"Leo kabila moja limekatiliwa mbali na
Israeli. 7 [h]Sasa tutawezaje kuwapa mabinti
zetu wawe wake zao kwa hao waliobaki
maadamu tumeapa kwa BWANA kuwa
hatutawapa binti zetu kuwa wake zao?"
8 [i]Ndipo wakasema, "Ni kabila lipi la Israeli
ambalo halikufika mbele za BWANA huko
Mispa?" Wakagundua kuwa hakuna hata
mmoja aliyetoka Yabeshi-Gileadi aliyefika
kambini kwa ajili ya kusanyiko la mkutano.
9 Walipohesabu waliona hakuna mtu yeyote
wa Yabeshi-Gileadi aliyekuwepo.

10 Ndipo mkutano wakatuma askari
12,000 na wakawaamuru kwenda Yabeshi-
Gileadi na kuwaua wale wote waishio
huko, walikuwepo wake na watoto.
11 [j]Wakasema, "Hilo ndilo mtakalofanya.
Ueni kila mtu mume na mke ambaye si
bikira." 12 [k]Wakakuta kati ya watu walioishi
Yabeshi-Gileadi wanawali mia nne ambao
hawajakutana kimwili na mwanaume, nao
wakawachukua kwenye kambi huko Shilo
katika nchi ya Kanaani.

13 [l]Ndipo mkutano ukatuma ujumbe wa
amani kwa Wabenyamini huko katika
mwamba wa Rimoni. 14 Basi Wabenyamini
wakarudi nyumbani mwao, wakapewa
wale wanawali wa Yabeshi-Gileadi
waliowaponya. Lakini hawakuwatosha
wanaume wote.

15 Waisraeli wakasikitika kwa ajili
ya Wabenyamini, kwa kuwa BWANA
ameweka ufa katika makabila ya Israeli.
16 Viongozi wa kusanyiko wakasema,
"Kwa kuwa wanawake wa Wabenyamini
wameangamizwa, tufanyeje ili kuwapatia
wake wale wanaume waliosalia? 17 Wale
waliopona wa Wabenyamini ni lazima
tuwape wake, ili wawe na warithi, ili kabila
lolote katika Israeli lisifutike. 18 [m]Hatuwezi
kuwapa binti zetu kuwa wake, kwa kuwa

[a]**20:44** 1Sam 10:26; Za 76:5
[b]**20:45** Yos 15:32; Amu 21:13
[c]**20:46** 1Sam 9:21
[d]**20:48** Amu 21:23
[e]**21:1** Yos 9:18; 11:3; Amu 20:1
[f]**21:4** Amu 20:26; 2Sam 24:25
[g]**21:5** Amu 5:23; 20:1
[h]**21:7** Yos 9:18
[i]**21:8** 1Sam 11:1; 31:11; 2Sam 2:4; 21:1; 1Nya 10:11
[j]**21:11** Hes 31:7; 31:17-18
[k]**21:12** Yos 18:1
[l]**21:13** Kum 2:28; Yos 15:35; Kum 20:10; Amu 20:47
[m]**21:18** Yos 9:18

sisi Waisraeli tumeapa kiapo hiki: 'Alaaniwe
mtu yeyote ampaye Mbenyamini mke.' "
19 [a]Ndipo waliposema, "Tazama iko sikukuu
ya kila mwaka ya BWANA katika Shilo,
kaskazini ya Betheli na mashariki mwa ile
barabara itokayo Betheli kwenda Shekemu,
upande wa kusini wa Lebona."
20 Hivyo wakawaelekeza Wabenyamini
wakisema, "Nendeni mkajifiche kwenye
mashamba ya mizabibu, 21 [b]nanyi
mwangalie. Wasichana wa Shilo
watakapojiunga kwenye kucheza, ninyi
tokeni kwenye hayo mashamba ya mizabibu
na kila mmoja akamate mwanamke mmoja
toka miongoni mwa hao wasichana wa
Shilo na mwende nao katika nchi ya
Benyamini. 22 Baba zao au ndugu zao
waume watakapotulalamikia, tutawaambia,
'Kuweni wakarimu kwetu, nanyi mturuhusu
tuwe nao kwa kuwa hatukuweza kumpa
kila mtu mke tulipopigana. Lakini ninyi pia
hamna hatia, kwa kuwa hamkuwapa wao
binti zenu kuwa wake.' "
23 [c]Basi hivyo ndivyo Wabenyamini
walivyofanya. Wakati wasichana
walipokuwa wakicheza, kila mtu
akamkamata msichana mmoja akamchukua
akaenda naye ili awe mke wake. Kisha
wakarudi katika urithi wao na kuijenga
upya miji na kuishi humo.
24 Wakati huo Waisraeli wakaondoka
sehemu ile na kwenda nyumbani kwao,
kwenye makabila yao na kwa jamaa zao,
kila mmoja kwenye urithi wake mwenyewe.
25 [d]Katika siku hizo kulikuwa hakuna
mfalme katika Israeli; kila mtu alifanya
kile alichoona ni sawa machoni pake
mwenyewe.

---

[a]**21:19** Yos 18:1; 1Sam 1:3; Yos 16:1; 16:1; 17:7
[b]**21:21** Kut 15:20; Amu 11:34
[c]**21:23** Yos 24:28; Amu 20:48
[d]**21:25** Kut 12:8; Amu 17:6

# RUTHU

*Naomi Na Ruthu*

1 [a]Wakati Waamuzi walipotawala Israeli,
kulikuwa na njaa katika nchi. Mtu mmoja
kutoka nchi ya Bethlehemu ya Yuda, pamoja
na mke wake na wanawe wawili, akaenda
kuishi katika nchi ya Moabu. 2 [b]Mtu huyu
aliitwa Elimeleki, mkewe aliitwa Naomi,
na hao wanawe wawili waliitwa Maloni
na Kilioni. Walikuwa Waefrathi kutoka
Bethlehemu ya Yuda. Wakaenda katika
nchi ya Moabu, wakaishi huko.
3 Elimeleki mumewe Naomi akafa, hivyo
Naomi akabaki na wanawe wawili. 4 [c]Nao
wakaoa wanawake Wamoabu, jina la mmoja
aliitwa Orpa, na wa pili aliitwa Ruthu.
Baada ya kama miaka kumi, 5 [d]Maloni na
Kilioni pia wakafa. Basi Naomi akabaki
hana mume wala wanawe wawili.
6 [e]Aliposikia akiwa huko Moabu kwamba
Bwana amewasaidia watu wake kwa
kuwapa chakula, Naomi na wakweze
wakajiandaa kurudi nyumbani. 7 Yeye
na wakweze wawili wakaondoka pale
walipokuwa wakiishi na kushika njia kurudi
nchi ya Yuda.
8 [f]Ndipo Naomi akawaambia wale wakwe
zake wawili, "Rudini, kila mmoja wenu
nyumbani kwa mama yake. Bwana na
awatendee fadhili kama mlivyowatendea
hao waliofariki, na pia mimi. 9 [g]Bwana na
amjalie kila mmoja wenu maisha mema
nyumbani kwa mume mwingine."
Kisha akawabusu, nao wakalia kwa sauti
kubwa, 10 wakamwambia, "Tutarudi pamoja
na wewe nyumbani kwa watu wako."
11 [h]Lakini Naomi akasema, "Rudini
nyumbani, binti zangu. Kwa nini mnifuate?
Je, mimi nitaweza tena kuwa na wana
wengine ambao wataweza kuwaoa ninyi?
12 Rudini nyumbani, binti zangu; mimi ni
mzee kiasi kwamba siwezi kumpata mume
mwingine. Hata kama ningefikiria kuwa
bado kuna tumaini kwangu, hata kama
ningekuwa na mume usiku huu na kuwazaa
wana, 13 [i]je, mngesubiri mpaka wakue?
Mngebakia bila kuolewa mkiwasubiri?
La, hasha, binti zangu. Nimepata uchungu
kuliko ninyi, kwa sababu mkono wa Bwana
umekuwa kinyume nami!"
14 [j]Kisha wakalia tena kwa sauti. Orpa
akambusu mama mkwe wake, akaenda
zake, lakini Ruthu akaambatana naye.
15 [k]Naomi akamwambia, "Tazama,
mwenzako anarejea kwa watu wake na kwa
miungu yake. Rudi pamoja naye."
16 [l]Lakini Ruthu akajibu, "Usinisihi
nikuache au niache kukufuata.
Utakakokwenda nami nitakwenda, na
wewe utakapoishi nitaishi. Watu wako
watakuwa watu wangu, na Mungu wako
atakuwa Mungu wangu. 17 [m]Pale utakapofia
nami nitafia hapo, na papo hapo nitazikwa.
Bwana na aniadhibu vikali, kama kitu
kingine chochote kitanitenga nawe
isipokuwa kifo." 18 [n]Naomi alipotambua
kwamba Ruthu amenuia kufuatana naye,
hakuendelea kumsihi tena.

---

[a]**1:1** Amu 2:16-18; Mwa 12:10; 35:19; 36:35; 47:4; 2Fal 6:25; Hag 1:11; Za 105:16; Kum 28:38; 1Fal 18:2; Mik 5:2
[b]**1:2** Rut 2:1; 4:3; Amu 3:30; 1Sam 16:18; Mwa 35:16-19
[c]**1:4** 1Fal 11:1; Mt 1:5; Rut 4:13; Ezr 9:2; Neh 13:23
[d]**1:5** Rut 2:11
[e]**1:6** Mwa 11:31; 36:35; 38:16; 50:24; Kut 4:31; Yer 29:10; Sef 2:7; Za 80:14; Zek 10:3; Lk 1:68; 7:16; Mwa 28:20; 48:15; Mit 30:8; Isa 55:10; Mt 6:11; Za 132:15
[f]**1:8** Mwa 38:11; 19:19; Yos 24:25; 2Tim 1:16
[g]**1:9** Rut 3:1; Mwa 27:27, 38; 29:11; Hes 25:6
[h]**1:11** Mwa 38:11; Kum 25:5
[i]**1:13** Mwa 38:11; Kut 1:14; 15:23; 1Sam 30:6; Ay 19:21; Za 32:4; 38:2; Amu 2:15; 4:5
[j]**1:14** Rut 2:11; 3:1; Mik 7:6; Mit 17:17; 18:24; Yn 6:66-69; Ebr 10:39; Mwa 31:28; Kum 10:20
[k]**1:15** Kum 25:7; Yos 24:14; Amu 11:24
[l]**1:16** 2Fal 2:2; Yos 24:15; Mwa 24:58; Za 45:10; Rut 2:11-12
[m]**1:17** 1Sam 3:17; 14:44; 20:13; 25:22; 1Fal 2:23; 19:2; 20:10; 2Sam 3:9; 19:13; 2Fal 6:31; 15:21
[n]**1:18** Mdo 21:14

19 [a]Kwa hiyo hao wanawake wawili
wakaondoka, wakafika Bethlehemu.
Walipofika Bethlehemu, mji mzima
ulitaharuki, wanawake wakashangaa,
wakasema, "Huyu aweza kuwa ni Naomi?"
20 [b]Akawaambia, "Msiniite tena Naomi,[c]
niiteni Mara,[d] kwa sababu Mwenyezi[e]
amenitendea mambo machungu sana.
21 [f]Mimi niliondoka hali nimejaa, lakini
BWANA amenirudisha mtupu. Kwa nini
kuniita Naomi? BWANA amenitendea
mambo machungu; Mwenyezi ameniletea
msiba."
22 [g]Kwa hiyo Naomi alirudi pamoja na
Ruthu Mmoabu mkwe wake, nao wakafika
Bethlehemu mwanzoni mwa kuvuna shayiri.

*Ruthu Akutana Na Boazi*

2 [h]Basi Naomi alikuwa na jamaa wa
upande wa mume wake, kutoka ukoo
wa Elimeleki, mtu maarufu ambaye aliitwa
Boazi.
2 [i]Ruthu, Mmoabu, akamwambia Naomi,
"Nitakwenda mashambani nikaokote
mabaki ya nafaka nyuma ya yule
nitakayepata kibali machoni pake."
Naomi akamwambia, "Nenda, binti
yangu." 3 [j]Basi akaenda, akaokota mabaki
ya nafaka mashambani nyuma ya wavunaji.
Ikatokea kwamba alijikuta anafanya kazi
kwenye shamba lililokuwa mali ya Boazi,
ambaye alitoka kwenye ukoo wa Elimeleki.
4 [k]Papo hapo Boazi akarudi kutoka
Bethlehemu, akawasalimu wavunaji,
akasema, "BWANA awe nanyi!"
Nao wakamjibu, "BWANA akubariki."
5 Boazi akamuuliza msimamizi wa
wavunaji, "Je, yule mwanamwali ni wa
nani?"
6 [l]Msimamizi akamjibu, "Ni yule Mmoabu
aliyerudi kutoka nchi ya Moabu pamoja
na Naomi. 7 [m]Yeye aliomba, 'Tafadhali
niruhusu niokote na kukusanya miongoni
mwa miganda nyuma ya wavunaji.' Naye
ameshinda shambani tangu asubuhi pasipo
kupumzika, isipokuwa kwa muda mfupi
kivulini."
8 Kisha Boazi akamwambia Ruthu,
"Binti yangu, nisikilize. Usiende kuokota
mabaki ya mavuno katika shamba lingine,
na usiondoke hapa. Kaa hapa na hawa
watumishi wangu wa kike. 9 Angalia
shamba wanaume wanamovuna, ufuate
nyuma yao. Nimewaamuru wanaume
hawa wasikuguse. Wakati wowote ukiona
kiu, nenda kwenye mitungi ukanywe maji
waliyoyateka wanaume hawa."
10 [n]Kwa ajili ya hili, akasujudu mpaka
nchi, akamwambia, "Jinsi gani nimepata
kibali machoni pako, hata ukanijali mimi
mgeni?"
11 [o]Boazi akamjibu, "Nimeambiwa
yote uliyomtendea mama mkwe wako
tangu mume wako alipofariki, na jinsi
ulivyomwacha baba yako na mama yako na
nchi yako ulimozaliwa, ukaja kuishi na watu
ambao hukuwafahamu awali. 12 [p]BWANA na
akulipe kwa yale uliyoyatenda. Ubarikiwe
kwa wingi na BWANA, Mungu wa Israeli,
ambaye umekimbilia mabawani mwake."
13 [q]Kisha Ruthu akasema, "Naomba
niendelee kupata kibali machoni pako,
bwana wangu. Kwa maana umenifariji na

[a]**1:19** Amu 17:7; Isa 23:7; Mt 21:10; Mao 2:15
[b]**1:20** Mwa 15:1; 17:1; Za 91:1; Kut 6:3; Ay 6:4
[c]20 Naomi maana yake Wa Kupendeza, Wa Kufurahisha.
[d]20 Mara maana yake Chungu.
[e]20 Mwenyezi hapa ina maana ya Shaddai kwa Kiebrania.
[f]**1:21** Ay 1:21; 30:11; Za 88:7; Isa 53:4
[g]**1:22** Rut 2:2-6, 21; 4:5, 10; Kut 9:31; Mwa 11:31; Law 19:9; 2Sam 21:9
[h]**2:1** Rut 2:3; 4:21; Mit 7:4; 1Sam 9:1; 1Fal 11:28; 1Nya 2:12; Mt 1:5; Lk 3:32
[i]**2:2** Rut 1:22; Law 19:9; 23:22; Mwa 6:8; 18:3; Kum 24:19
[j]**2:3** 2Fal 4:18; Yer 9:22; Amo 9:13
[k]**2:4** Lk 1:28; Mwa 28:3; 2The 3:16; 2Tim 4:22; Kol 4:6; Hes 6:24; Amu 6:12; Za 129:7-8
[l]**2:6** Rut 1:22
[m]**2:7** Mwa 37:7; Law 19:9; 2Sam 4:5
[n]**2:10** Mwa 19:1; 31:15; 1Sam 25:23; 20:41; Kum 15:3
[o]**2:11** Rut 1:5, 14, 16-17; Isa 55:5; Mit 31:31; Rut 1:14; Lk 5:11, 28; 14:33; 18:29, 30
[p]**2:12** 1Sam 24:19; 26:23-25; Za 17:8; 18:20; 36:7; 57:1; 61:4; 63:7; 91:4; 71:1; Mit 25:22; Yer 31:16; Yos 24:15
[q]**2:13** Mwa 18:3; Flp 2:3; 1Sam 25:41

umezungumza kwa ukarimu na mjakazi wako, hata ingawa mimi si bora kama mmoja wa watumishi wako wa kike.”

14 [a]Wakati wa chakula, Boazi akamwambia Ruthu, “Karibia hapa. Kula mkate na uchovye ndani ya siki.”

Alipoketi pamoja na wavunaji, akampa nafaka zilizookwa. Akala kiasi alichotaka na kusaza. 15 [b]Alipoinuka ili kuokota mabaki ya nafaka, Boazi akawaagiza watu wake, “Hata kama atakusanya kati ya miganda, msimzuie. 16 [c]Badala yake, toeni masuke katika miganda, mwachieni ayaokote, na msimkemee.”

17 [d]Basi Ruthu akaokota masazo shambani hata jioni. Akatwanga ile shayiri aliyokusanya, ikajaa efa moja.[e] 18 Akaibeba na kuelekea mjini, naye mama mkwe wake akaona jinsi alivyoweza kuokota nafaka nyingi. Pia Ruthu akachukua kile alichobakiza baada ya kula na kushiba, akampa.

19 Basi mkwewe akamuuliza, “Je, umeokota wapi leo? Umefanya kazi wapi? Abarikiwe mtu yule aliyekujali.”

Ndipo Ruthu akamwambia mama mkwe wake juu ya yule ambaye yeye alikuwa amefanyia kazi katika shamba lake. Akasema, “Yule mtu niliyefanyia kazi kwake leo, anaitwa Boazi.”

20 [f]Naye Naomi akamwambia mkwewe, “Bwana ambariki! Hakuacha kuonyesha fadhili zake kwa walio hai na kwa waliokufa.” Pia akamwambia, “Huyo mtu ni mmoja wa jamaa yetu wa karibu anayestahili kutukomboa.”

21 [g]Kisha Ruthu, Mmoabu, akasema, “Hata aliniambia, ‘Kaa pamoja na watumishi wangu mpaka watakapomaliza kuvuna nafaka yangu yote.’ ”

22 Kisha Naomi akamwambia Ruthu mkwewe, “Binti yangu, itakuwa vyema wewe ufuatane na wasichana wake, kwa sababu katika shamba la mtu mwingine wanaweza kukudhuru.”

23 [h]Kwa hivyo Ruthu akafuatana na watumishi wa kike wa Boazi, akaokota mpaka mwisho wa mavuno ya shayiri na ya ngano. Naye aliishi na mama mkwe wake.

*Ruthu Na Boazi Kwenye Sakafu Ya Kupuria*

3 [i]Kisha Naomi akamwambia mkwewe, “Binti yangu, je, nisingelikutafutia pumziko ambako utatunzika vyema? 2 [j]Je, Boazi, ambaye umekuwa pamoja na watumishi wake wasichana, si jamaa yetu wa karibu? Usiku wa leo atakuwa anapepeta ngano kwenye sakafu ya kupuria. 3 [k]Basi oga na ukajipake marashi, ujivalie nguo zako nzuri. Kisha uende kwenye sakafu ya kupuria, lakini angalia asijue kwamba upo pale mpaka atakapomaliza kula na kunywa. 4 Atakapokwenda kulala, angalia mahali atakapolala. Kisha uende ufunue miguu yake, ulale. Naye atakuambia utakalofanya.”

5 [l]Ruthu akajibu, “Lolote usemalo nitatenda.” 6 [m]Basi akashuka mpaka kwenye sakafu ya kupuria, akafanya kila kitu mama mkwe wake alichomwambia kufanya.

7 [n]Wakati Boazi alipomaliza kula na kunywa, naye akawa amejawa na furaha, alikwenda kulala mwisho wa lundo la nafaka. Ruthu akanyemelea polepole, akafunua miguu yake, na akalala. 8 Usiku wa manane, kitu kilimshtua Boazi, akajigeuza, akagundua yupo mwanamke amelala miguuni pake.

---

[a]**2:14** Mwa 3:19; Law 23:14
[b]**2:15** Mwa 37:7; Law 19:9
[c]**2:16** Mwa 37:10
[d]**2:17** Amu 6:11; Law 19:36
[e]17 Efa moja ni sawa na kilo 22.
[f]**2:20** Amu 17:2; 1Sam 23:21; Mwa 11:31; 19:19; 2Sam 2:5; Ay 29:13; 2Tim 1:16; Mit 17:17; Law 25:25; Rut 3:9; 4:1, 14
[g]**2:21** Rut 1:22
[h]**2:23** Kut 9:31; Mwa 30:14; 1Sam 6:13; Kum 16:9
[i]**3:1** Rut 1:9, 14, 19; 1Kor 7:36; 1Tim 5:8; Kum 4:40; Za 128:2; Yer 22:15, 16
[j]**3:2** Rut 2:1, 8; Law 2:14; Hes 18:27; Amu 6:11
[k]**3:3** 2Sam 12:20; 14:2; 2Fal 5:10; Za 26:6; 51:2; Isa 1:16; 61:3; Yer 4:14; Eze 16:9; Mwa 41:14; Kut 32:6; Mhu 2:3; Yer 15:17
[l]**3:5** Efe 6:1; Kol 3:20
[m]**3:6** Hes 18:27
[n]**3:7** Amu 19:6; 1Sam 25:36; 2Sam 13:28; 1Fal 21:7; Es 1:10; Wim 7:2; 2Nya 31:6; Yer 50:26; Hag 2:16

9 [a]Akauliza, “Wewe ni nani?”
Akajibu, “Ni mimi Ruthu, mjakazi
wako. Uitande nguo yako juu yangu, kwa
sababu wewe ndiwe jamaa wa karibu wa
kutukomboa.”
10 [b]Akamwambia, “Binti yangu, ubarikiwe
na BWANA. Wema huu wa sasa ni mkuu
kushinda hata ule ulioonyesha mwanzoni.
Hukuwakimbilia vijana, wakiwa matajiri
au maskini. 11 [c]Sasa, binti yangu, usiogope.
Nitakufanyia yote uliyoomba. Kwa maana
mji wote wa watu wangu wanakujua ya
kwamba wewe ni mwanamke mwenye tabia
nzuri. 12 [d]Ingawa ni kweli kwamba mimi
ndiye jamaa aliye karibu, bado kuna mtu
mwingine wa jamaa aliye karibu zaidi wa
kukomboa kuliko mimi. 13 [e]Wewe kaa hapa
usiku huu, kisha asubuhi kama akikubali
kukomboa, vyema na akomboe. La sivyo
kama hayuko tayari, hakika kama BWANA
aishivyo nitafanya hivyo. Lala hapa mpaka
asubuhi.”
14 [f]Hivyo huyo mwanamke akalala
miguuni pake mpaka asubuhi, akaondoka
mapema pasipo mtu kuweza kumtambua
mwenzake, maana Boazi alisema,
“Isijulikane kabisa ya kuwa mwanamke
alifika kwenye sakafu ya kupuria.”
15 [g]Pia akamwambia, “Leta shela yako
uliyoivaa, uitandaze.” Naye alipoitandaza,
akamimina vipimo sita vya shayiri,
akamtwika. Kisha Ruthu akarudi zake
mjini.
16 Basi Ruthu alipofika kwa mama mkwe
wake Naomi, akamuuliza, “Je, binti yangu,
ilikuwaje huko?”
Ndipo akamwelezea kila kitu Boazi
alichomfanyia. 17 Akaendelea kusema,
“Amenipa shayiri vipimo sita[h] akisema,
‘Usiende kwa mama mkwe wako mikono
mitupu.’ ”
18 [i]Kisha Naomi akasema, “Subiri binti
yangu, mpaka utakapojua kwamba hili
jambo limekwendaje. Kwa sababu mtu
huyu hatatulia mpaka akamilishe jambo
hili leo.”

*Boazi Amwoa Ruthu*

4 [j]Boazi akakwea mpaka kwenye lango la
mji, akaketi pale. Yule mtu wa jamaa
aliyekuwa wa karibu wa kukomboa, ambaye
Boazi alimtaja, akaja. Boazi akasema, “Njoo
hapa, rafiki yangu. Karibu uketi.” Naye
akakaribia, akaketi.
2 [k]Boazi akatwaa watu kumi miongoni
mwa wazee wa mji, akawaambia, “Ketini
hapa.” Nao wakaketi. 3 [l]Kisha akamwambia
yule jamaa wa karibu wa kukomboa,
“Naomi, aliyerudi hapa kutoka nchi ya
Moabu, anauza sehemu ya ardhi iliyokuwa
mali ya ndugu yetu Elimeleki. 4 [m]Nami
niliwaza nikujulishe wewe na kukuambia
uinunue mbele ya hawa waliopo hapa, na
mbele ya wazee wa watu wangu. Kama
wewe utaikomboa, haya fanya hivyo.
Lakini kama hutaikomboa, uniambie, ili
nijue. Kwa kuwa hakuna mtu mwingine
mwenye haki ya kuikomboa ila wewe na
baada yako ni mimi.”
Naye akasema, “Nitaikomboa mimi.”
5 [n]Ndipo Boazi akasema “Siku
utakaponunua hiyo ardhi kutoka kwa
Naomi na Ruthu, Mmoabu, itakubidi
kumchukua pia huyo mjane, ili kudumisha
jina la marehemu pamoja na mali yake.”
6 [o]Aliposikia hili, yule jamaa wa karibu wa
kukomboa akasema, “Basi mimi sitaweza
kuikomboa, kwa sababu inaonekana

---

[a]**3:9** Eze 16:8; Rut 2:20
[b]**3:10** Amu 17:2; Yos 2:12
[c]**3:11** Mit 12:4; 14:1; 31:10
[d]**3:12** Rut 2:20; 4:1
[e]**3:13** Kum 25:5; Rut 4:5, 6; Mt 22:24; Amu 8:19; Yer 4:2; Ebr 6:16; Hes 14:21; Hos 4:15
[f]**3:14** Hes 18:27; Rum 14:16; 2Kor 8:21; Rum 12:17; 14:16; 2Kor 8:21; 1The 5:22; 1Pet 2:12
[g]**3:15** Isa 3:22
[h]17 Vipimo sita vya shayiri ni sawa na kilo 15.
[i]**3:18** Za 37:3-5
[j]**4:1** Mwa 18:1; 23:10; Rut 2:20; 3:12
[k]**4:2** Kut 3:16; 18:21, 22; Kum 16:18; 17:9; 29:10; 25:7; 1Fal 21:8; Za 82:2; Mit 31:21, 23
[l]**4:3** Law 25:25; Rut 1:2
[m]**4:4** Law 25:25; Rum 12:17; 2Kor 8:21; Flp 4:8; Mwa 23:18; Yer 32:7-8
[n]**4:5** Rut 1:22; 3:13; Mwa 38:8; Kum 25:5-6; Mt 22:24
[o]**4:6** Law 25:25; Rut 3:13; Kum 25:7

nitauhatarisha urithi wangu. Wewe
ikomboe mwenyewe. Mimi sitaweza.”
7 [a](Basi katika siku za kale huko Israeli,
ili kukamilisha tendo la kukomboa na
kukabidhiana mali, mmoja huvua kiatu
chake na kumpatia mwingine. Hii ilikuwa
ni njia ya kuhalalisha mabadilishano katika
Israeli.)
8 [b]Basi yule jamaa wa karibu wa
kukomboa akamwambia Boazi, “Wewe
inunue mwenyewe.” Naye huyo jamaa
akavua kiatu chake.
9 [c]Kisha Boazi akawatangazia wazee
na watu wote waliokuwepo, “Leo ninyi
ni mashahidi kwamba mimi nimenunua
kutoka kwa Naomi yote yaliyokuwa
mali ya Elimeleki, Kilioni na Maloni.
10 [d]Nimemchukua pia Ruthu, Mmoabu,
mjane wa Maloni, awe mke wangu, ili
kuendeleza jina la marehemu pamoja na
mali zake, ili jina lake marehemu lisitoweke
miongoni mwa jamaa yake, wala katika
kumbukumbu za mji wake. Leo hivi ninyi
ni mashahidi!”
11 [e]Kisha wazee pamoja na watu wote
waliokuwa langoni wakasema, “Sisi ni
mashahidi. BWANA na amfanye mwanamke
huyu aingiaye nyumbani mwako kuwa
kama Raheli na kama Lea, wale wanawake
wawili ambao pamoja waliijenga nyumba
ya Israeli. Nawe ufanikiwe katika Efrathi
na uwe mashuhuri katika Bethlehemu.
12 [f]Kupitia kwa watoto ambao BWANA
atakupa kutokana na huyu mwanamwali,
jamaa yako na ifanane na ya Peresi, ambaye
Tamari alimzalia Yuda.”

*Wazao Wa Boazi*

13 [g]Basi Boazi akamwoa Ruthu, naye
akawa mke wake. Alipoingia kwake, BWANA
akamjalia Ruthu, naye akapata mimba,
akamzaa mtoto wa kiume.
14 [h]Wanawake
wakamwambia Naomi: “Ahimidiwe BWANA,
asiyekuacha bila kuwa na jamaa wa karibu
wa kukomboa. Na awe mashuhuri katika
Israeli yote!
15 [i]Atakurejeshea uhai wako
na kukuangalia katika siku za uzee wako.
Kwa maana mkweo ambaye anakupenda,
na ambaye kwako ni bora zaidi ya watoto
wa kiume saba, ndiye alimzaa.”
16 Basi Naomi akamchukua yule mtoto,
akampakata na akawa mlezi wake.
17 [j]Wanawake waliokuwa jirani zake
wakasema, “Naomi ana mtoto wa kiume.”
Wakamwita jina lake Obedi. Yeye ndiye
baba yake Yese, aliye baba yake Daudi.
18 [k]Hivi ndivyo vizazi vya Peresi:

Peresi alimzaa Hesroni,
19 [l]Hesroni akamzaa Ramu,
Ramu akamzaa Aminadabu,
20 [m]Aminadabu akamzaa Nashoni,
Nashoni akamzaa Salmoni,
21 [n]Salmoni akamzaa Boazi,
Boazi akamzaa Obedi,
22 Obedi akamzaa Yese,
na Yese akamzaa Daudi.

[a] **4:7** Law 25:24; Isa 8:1-2, 16-20; Kum 25:7-9
[b] **4:8** Kum 25:9
[c] **4:9** Isa 8:2; Yer 32:10, 44
[d] **4:10** Rut 1:22; Kum 25:5-6; Yos 24:22
[e] **4:11** Mwa 4:19; 23:10; 29:16; 35:16; Kum 25:9; Rut 1:19; Za 127:3
[f] **4:12** 1Nya 2:4; Mt 1:3; 1Sam 2:20; Mwa 38:6, 24, 29
[g] **4:13** Mwa 8:1; 29:31-32; 33:5; 30:6; Lk 1:57
[h] **4:14** Lk 1:58; Rum 12:15; Mwa 24:27; Rut 2:20
[i] **4:15** Mwa 11:31; Isa 1:8; 2:5; Ay 1:2
[j] **4:17** 1Sam 16:1, 13, 18; 17:12, 17, 58; 1Nya 2:12-15; Za 72:20
[k] **4:18** Mwa 38:29; Hes 26:21
[l] **4:19** Kut 6:23
[m] **4:20** Hes 1:7; 7:12
[n] **4:21** Rut 1:2; Mt 1:21

# 1 SAMWELI

*Kuzaliwa Kwa Samweli*

**1** [a]Kulikuwepo na mtu mmoja kutoka Rama, Msufi kutoka nchi ya vilima vya Efraimu, ambaye jina lake aliitwa Elikana mwana wa Yerohamu, mwana wa Elihu mwana wa Tohu, mwana wa Sufu, Mwefraimu. 2 [b]Alikuwa na wake wawili, mmoja aliitwa Hana na mwingine Penina. Penina alikuwa na watoto, lakini Hana hakuwa na mtoto.

3 [c]Kila mwaka mtu huyu alikwea kutoka mji wake ili kuabudu na kutoa dhabihu kwa Bwana Mwenye Nguvu Zote huko Shilo, ambapo Hofni na Finehasi, wana wawili wa Eli, walikuwa makuhani wa Bwana. 4 [d]Kila mara ilipofika siku ya Elikana kutoa dhabihu, aliwapa mafungu Penina mkewe na wanawe wote pamoja na binti zake. 5 [e]Lakini alimpa Hana fungu maradufu kwa sababu alimpenda, ingawa Bwana alikuwa amemfunga tumbo. 6 [f]Kwa sababu Bwana alikuwa amemfunga tumbo, mke mwenzake alikuwa anamchokoza ili kumuudhi. 7 [g]Hili liliendelea mwaka baada ya mwaka. Kila mara Hana alipokwenda katika nyumba ya Bwana, mke mwenzake alikuwa akimkasirisha mpaka analia na kushindwa kula. 8 [h]Elikana mumewe akawa anamwambia, "Hana, kwa nini unalia? Kwa nini huli? Kwa nini kuvunjika moyo? Je, mimi si bora zaidi kwako kuliko watoto kumi?"

9 [i]Siku moja walipokuwa wamemaliza kula na kunywa huko Shilo, Hana alisimama. Wakati huo kuhani Eli alikuwa ameketi kwenye kiti pembeni mwa mwimo wa mlango wa Hekalu la Bwana. 10 [j]Kwa uchungu wa rohoni Hana alilia sana na akamwomba Bwana. 11 [k]Naye akaweka nadhiri, akisema, "Ee Bwana Mwenye Nguvu Zote, laiti ungeangalia huzuni kuu ya mtumishi wako na kunikumbuka mimi, wala usimsahau mtumishi wako nawe ukampa mwana, basi huyo mwana nitamtoa kwa Bwana kwa siku zote za maisha yake, wala wembe hautapita kichwani mwake."

12 Alipokuwa anaendelea kumwomba Bwana, Eli alichunguza kinywa chake. 13 Hana alikuwa akiomba moyoni mwake, midomo yake ikiwa inachezacheza lakini sauti haikusikika. Eli akafikiri alikuwa amelewa 14 naye akamwambia, "Utaendelea kulewa mpaka lini? Achilia mbali mvinyo wako."

15 [l]Hana akajibu, "Si hivyo bwana wangu, mimi ni mwanamke mwenye huzuni kubwa. Mimi sijanywa mvinyo wala kileo, nilikuwa ninaumimina moyo wangu kwa Bwana. 16 [m]Usimdhanie mtumishi wako kuwa mwanamke mwovu; nimekuwa nikiomba hapa katika wingi wa uchungu mkuu na huzuni."

17 [n]Eli akamjibu, "Nenda kwa amani, naye Mungu wa Israeli na akujalie kile ulichomwomba."

18 [o]Hana akasema, "Mtumishi wako na apate kibali machoni pako." Kisha akaondoka zake na kula chakula, wala uso wake haukuwa na huzuni tena.

---

[a]**1:1** Mwa 18:25; 1Sam 9:5; Yos 17:17-18; 21:20-22; 1Nya 6:27-34; Rut 1:2
[b]**1:2** Mwa 4:19; Kum 21:15-17
[c]**1:3** Kut 23:14; 1Sam 2:19; 20:6; Lk 2:41; Kum 12:5-7; 1Sam 2:31; 14:3; Yos 18:1; Amu 18:31; Za 78:60; Yer 7:12-14
[d]**1:4** Law 7:15-18; Kum 12:17-18; Mwa 29:34
[e]**1:5** Mwa 37:3; 11:30; 29:31
[f]**1:6** Mwa 16:4-5
[g]**1:7** 2Sam 12:17; Za 102:4; Kut 23:14; Kum 16:16; Kut 23:14
[h]**1:8** Rut 4:15
[i]**1:9** 1Sam 3:3
[j]**1:10** Ay 3:20; 7:11; 10:1; 21:25; 23:2; 27:2; Isa 38:15; Yer 20:18
[k]**1:11** Amu 11:30; 13:7; 13:5; Lk 1:15; Mwa 17:1; 8:1; Za 24:10; 46:7; Isa 1:9; Hes 6:1-21; 21:2; 30:3-8; Mhu 5:4; Mwa 29:32; Kut 4:31
[l]**1:15** 2Fal 4:27; Za 42:4; 62:8; Mao 2:19
[m]**1:16** Za 55:2; 2Kor 6:15
[n]**1:17** Hes 6:26; 1Sam 20:42; 2Fal 5:19; Mdo 15:33; Mwa 25:21; Za 20:3-5; Mwa 33:15; Yn 16:24
[o]**1:18** Mwa 18:3; Rut 2:13; Rum 15:13; Ufu 2:13; Mhu 9:7

19 [a]Kesho yake asubuhi na mapema
waliamka wakaabudu mbele za BWANA
na kisha wakarudi nyumbani kwao huko
Rama. Elikana akakutana kimwili na
mkewe Hana, naye BWANA akamkumbuka.
20 [b]Hivyo wakati ulipotimia, Hana akapata
mimba na akamzaa mwana. Hana akamwita
jina lake Samweli, akasema, "Kwa kuwa
nilimwomba kwa BWANA."

*Hana Anamweka Samweli Wakfu*

21 [c]Wakati huyo mtu Elikana alipanda
pamoja na jamaa yake yote kutoa dhabihu
ya mwaka kwa BWANA na kutimiza nadhiri
yake, 22 [d]Hana hakwenda. Alimwambia
mume wake, "Baada ya mtoto kuachishwa
kunyonya, nitamchukua na kumpeleka
mbele za BWANA, naye ataishi huko wakati
wote."
23 [e]Elikana mumewe akamwambia, "Fanya
lile unaloona ni bora zaidi kwako. Ukae
hapa mpaka utakapomwachisha kunyonya,
BWANA na akujalie kutimiza nadhiri yako."
Hivyo huyo mwanamke akakaa nyumbani
na kumnyonyesha mwanawe mpaka
alipomwachisha kunyonya.
24 [f]Baada ya mtoto kuachishwa kunyonya,
Hana akamchukua huyo mtoto, akiwa
mdogo hivyo hivyo, pamoja na fahali wa
miaka mitatu, efa ya unga[g] na kiriba cha
divai, naye akamleta mtoto kwenye nyumba
ya BWANA huko Shilo. 25 Walipokwisha
kumchinja yule fahali, wakamleta mtoto
kwa Eli, 26 naye Hana akamwambia Eli,
"Hakika kama uishivyo, bwana wangu,
mimi ndiye yule mama ambaye alisimama
hapa karibu nawe akiomba kwa BWANA.
27 [h]Niliomba mtoto huyu, naye BWANA
amenijalia kile nilichomwomba. 28 [i]Hivyo
sasa ninamtoa kwa BWANA. Kwa maana
maisha yake yote atakuwa ametolewa kwa
BWANA." Naye akamwabudu BWANA huko.

*Maombi Ya Hana*

2 [j]Kisha Hana akaomba na kusema:

"Moyo wangu
wamshangilia BWANA,
katika BWANA pembe yangu
imeinuliwa juu.
Kinywa changu chajisifu juu ya adui
zangu,
kwa kuwa naufurahia wokovu
wako.

2 [k]"Hakuna yeyote aliye mtakatifu
kama BWANA,
hakuna mwingine zaidi yako;
hakuna Mwamba kama Mungu
wetu.

3 [l]"Msiendelee kusema kwa kiburi
hivyo
wala msiache vinywa vyenu
kunena kwa kiburi,
kwa kuwa BWANA ndiye Mungu
ajuaye,
na kwa yeye matendo hupimwa.

4 [m]"Pinde za mashujaa zimevunjika,
lakini wale wanaojikwaa
wamevikwa nguvu.
5 [n]Wale waliokuwa na chakula tele
wamejikodisha wenyewe
ili kupata chakula,
lakini wale waliokuwa na njaa
hawana njaa tena.
Mwanamke yule aliyekuwa tasa
amezaa watoto saba,

---

[a]**1:19** Yos 18:25; Mwa 8; 1; 29:31
[b]**1:20** Mwa 17:19; 29:32; 30:6; Kut 2:10; Mt 1:21; 1Sam 7:5; 12:23; 1Nya 6:27; Yer 15:1; Ebr 11:32
[c]**1:21** Mwa 28:20; Hes 30:2; Kum 12:11
[d]**1:22** Lk 2:22; Kut 13:2; 1Sam 2:11; 3:1
[e]**1:23** Mwa 25:21; 21:8; Hes 30:7; 2Sam 7:25
[f]**1:24** Hes 15:8-10
[g]24 Efa moja ya unga ni sawa na kilo 22.
[h]**1:27** 1Sam 2:20; Za 66:19-20; Mit 7:7
[i]**1:28** Amu 13:7; Mwa 24:26, 52
[j]**2:1** Lk 1:46-55; Za 13:5; 33:21; 18:2; 89:17; 148:4; 6:8; Hes 10:35; Zek 10:7; Flp 4:6
[k]**2:2** Kut 15:11; 8:10; 33:22; Law 11:44; Isa 40:25; 46:5; Mwa 49:25; Kum 32:37; 2Sam 22:2-32; 23:2-3; Za 31:3; 71:3
[l]**2:3** Za 17:10; 31:18; 73:8; 75:4; 94:4; Yos 22:22; 1Sam 16:7; 1Fal 8:39; 1Nya 28:9; 2Nya 6:30; Mit 15:11; 24:11-12; Yer 11:20; 17:16
[m]**2:4** 2Sam 1:27; Za 37:15; 46:9; 76:3; Ay 17:9; Isa 40:31; 41:1; 52:1; 57:10
[n]**2:5** Lk 1:53; Za 113:9; Isa 54:1; Yer 15:9; Gal 4:27

lakini yule ambaye alikuwa na wana
wengi
amedhoofika.

6 [a]"BWANA huua na huleta uhai,
hushusha chini mpaka kaburini[b] na
hufufua.
7 [c]BWANA humfanya mtu maskini
naye hutajirisha,
hushusha na hukweza.
8 [d]Humwinua maskini kutoka
mavumbini
na humwinua mhitaji kutoka
lundo la majivu;
huwaketisha pamoja na wakuu
na kuwafanya warithi kiti cha enzi
cha heshima.

"Kwa kuwa misingi ya dunia ni ya
BWANA;
juu yake ameuweka ulimwengu.
9 [e]Yeye atailinda miguu ya watakatifu
wake,
lakini waovu watanyamazishwa
kwenye giza.

"Si kwa nguvu mtu hushinda;
10 [f]wale wampingao BWANA
wataharibiwa kabisa.
Atapiga radi dhidi yao kutoka
mbinguni;
BWANA ataihukumu miisho ya
dunia.

"Atampa nguvu mfalme wake,
na kuitukuza pembe
ya mpakwa mafuta wake."

11 [g]Kisha Elikana akaenda nyumbani
Rama, lakini mtoto akahudumu mbele za
BWANA chini ya kuhani Eli.

*Wana Waovu Wa Eli*

12 [h]Wana wa Eli walikuwa watu wabaya
kabisa, hawakumheshimu BWANA. 13 [i]Basi
ilikuwa desturi ya makuhani pamoja na
watu kwamba kila mara yeyote anapotoa
dhabihu na huku nyama ikiwa inachemshwa,
mtumishi wa kuhani angalikuja na uma
wenye meno matatu mkononi mwake.
14 [j]Angeutumbukiza huo uma kwenye sufuria
au birika au sufuria kubwa au chungu,
naye kuhani angalijichukulia mwenyewe
chochote ambacho uma ungekileta. Hivi
ndivyo walivyowatendea Waisraeli wote
waliokuja Shilo. 15 Lakini hata kabla mafuta
ya mnyama hayajachomwa, mtumishi wa
kuhani angalikuja na kusema kwa mtu
ambaye alikuwa akitoa dhabihu, "Mpe
kuhani nyama akaoke, kwani hatapokea
nyama iliyochemshwa kutoka kwako, ila
iliyo mbichi tu."
16 [k]Kama mtu akimwambia, "Mafuta ya
mnyama na yachomwe kwanza, ndipo
uchukue chochote unachotaka," mtumishi
angalijibu, "Hapana, nipe sasa, kama
huwezi nitaichukua kwa nguvu."
17 [l]Hii Dhambi ya hawa vijana ilikuwa
kubwa sana machoni pa BWANA, kwa
kuwa waliitendea dhabihu ya BWANA kwa
dharau.
18 [m]Lakini Samweli alikuwa akihudumu
mbele za BWANA, kijana akivaa kisibau

[a]**2:6** Kum 32:39; Ay 5:18; Hos 6:1; Yn 5:25-29; 11:25, 26; Ufu 1:18
[b]6 Kaburini hapa maana yake ni Kuzimu, kwa Kiebrania ni Sheol.
[c]**2:7** Kum 8:18; Ay 5:11; 40:12; Za 75:7; Isa 2:12; 13:11; 22:19; Dan 4:37; Za 75:8
[d]**2:8** Za 113:7-8; 72:12; 107:41; 145:14; 146:8; 104:5; Mit 8:29; Mt 23:12; 2Sam 7:8; Ay 36:7; 15:7; 38:4; Isa 22:23; 40:12; Yer 10:12; Eze 21:26; Yak 2:5; 1Fal 16:2
[e]**2:9** Za 91:12; 121:3; Mit 3:26; 2:8; Ay 10:22; 37:4-5; 38:1; Za 18:13; 29:3; 96:13; 98:9; 18:1; 21:1; 59:16; 89:24; Kum 33:17; Lk 1:69; Isa 66:6; 5:30; 8:22; 59:9; 60:2; Yer 13:16; Amo 5:18-20; Sef 1:14-15; Mt 8:12; 25:31-32; 1Sam 17:47; 2Sam 22:14
[f]**2:10** Za 96:13
[g]**2:11** Yos 18:25; Hes 16:9; 1Sam 3:1; 2:18
[h]**2:12** Yer 2:8; 9:6; Kum 13:13; Rum 1:28
[i]**2:13** Kum 18:3; Law 7:29-36; 1Sam 2:12
[j]**2:14** Hes 15:30; Isa 22:14; Yer 7:16; Ebr 10:26-31
[k]**2:16** Law 3:3, 14-16; 7:29-34
[l]**2:17** Hes 14:11; Yer 7:21; Eze 22:26; Mal 2:7-9; 1Sam 2:22; Rut 1:17; Mt 26:63
[m]**2:18** 1Sam 22:18; 23:9; 2Sam 6:14; 1Nya 15:27; Mwa 18:25; 1Sam 16:10-12; Ay 1:21; 2:10; Za 39:9

cha kitani. 19 [a]Kila mwaka mama yake alimshonea joho dogo na kumchukulia wakati alipokwea pamoja na mumewe kutoa dhabihu ya mwaka. 20 [b]Eli alikuwa akiwabariki Elikana na mkewe, akisema, “Bwana na akupe watoto kwa mwanamke huyu ili kuchukua nafasi ya yule aliyekuwa amemwomba na akamtoa kwa Bwana.” Kisha wakawa wanakwenda nyumbani. 21 [c]Bwana akawa mwenye neema kwa Hana, naye akapata mimba akazaa wana watatu na binti wawili. Wakati huo, kijana Samweli akaendelea kukua mbele za Bwana.

22 [d]Basi Eli, ambaye alikuwa mzee sana, alisikia kuhusu kila kitu ambacho wanawe walikuwa wakiwafanyia Israeli wote na jinsi walivyokutana kimwili na wanawake waliohudumu kwenye ingilio la Hema la Kukutania. 23 Hivyo akawaambia, “Kwa nini mmefanya mambo kama haya? Nimesikia kutoka kwa watu wote juu ya haya matendo yenu maovu. 24 Sivyo, wanangu, hii si habari nzuri ambayo ninasikia ikienea miongoni mwa watu wa Bwana. 25 [e]Kama mtu akifanya dhambi dhidi ya mtu mwenzake, mtu mwingine aweza kumwombea kwa Mungu, lakini kama mtu akimfanyia Mungu dhambi, ni nani atakayemwombea?” Hata hivyo wanawe hawakusikia maonyo ya baba yao, kwa sababu Bwana alitaka kuwaua.

26 [f]Naye kijana Samweli akaendelea kukua katika kimo, akimpendeza Bwana na wanadamu.

### *Unabii Dhidi Ya Nyumba Ya Eli*

27 [g]Basi mtu wa Mungu akaja kwa Eli na kumwambia, “Hivi ndivyo asemavyo Bwana: ‘Je, sikujifunua waziwazi kwa nyumba ya baba yako wakati walikuwa huko Misri chini ya Farao? 28 [h]Nilimchagua baba yako kati ya makabila yote ya Israeli kuwa kuhani wangu, kukwea kwenye madhabahu yangu, kufukiza uvumba na kuvaa kisibau mbele yangu. Pia niliwapa nyumba ya baba yako sadaka zote zilizotolewa kwa moto na Waisraeli. 29 [i]Kwa nini unadharau dhabihu zangu na sadaka zile nilizoziamuru kwa ajili ya makao yangu? Kwa nini unawaheshimu wanao kuliko mimi kwa kujinenepesha wenyewe kwa kula sehemu zilizo bora za kila sadaka zinazotolewa na watu wangu wa Israeli?’

30 [j]“Kwa hiyo, Bwana, Mungu wa Israeli asema: ‘Niliahidi kuwa nyumba yako na nyumba ya baba yako wangehudumu mbele zangu milele.’ Lakini sasa Bwana anasema: ‘Jambo hili na liwe mbali nami! Wale wanaoniheshimu nitawaheshimu, wale wanaonidharau mimi watadharauliwa. 31 [k]Wakati unakuja nitakapozipunguza nguvu zenu na nguvu ya nyumba ya baba yenu, ili pasiwepo mtu katika mbari yenu atakayeishi kuuona uzee 32 [l]nanyi mtaona huzuni katika makao yangu. Ingawa Israeli watafanyiwa mema, katika mbari yenu kamwe hapatakuwepo mtu atakayeishi hadi kuwa mzee. 33 [m]Kila mmoja wenu ambaye sitamkatilia mbali kutoka madhabahuni pangu atabakizwa tu kupofusha macho yenu kwa machozi na kuihuzunisha mioyo yenu, nao wazao wenu wote watakufa watakapokuwa wamefikia umri wa kustawi.

34 [n]“ ‘Kile kitakachotokea kwa wanao wawili, Hofni na Finehasi, kitakuwa ishara kwako. Wote wawili watakufa katika siku

---

[a]**2:19** 1Sam 1:3; Mwa 18:25; 1Sam 18:14; 2Tim 4:22; 1Sam 9:6
[b]**2:20** 1Sam 1:27; Lk 2:34; Amu 20:1
[c]**2:21** Mwa 21:1; Amu 13:24; Lk 1:80; 2:40
[d]**2:22** Kut 38:8
[e]**2:25** Kut 4:21; 32:10; Yos 11:20; Hes 11:2; 1Sam 3:14; 1Fal 13:6; Ay 9:33; Za 106:30; Isa 1:18; 22:14; Yer 15:1; Ebr 10:26
[f]**2:26** Amu 13:24; Lk 2:52; Mit 3:4; Mdo 2:47; Rum 14:18
[g]**2:27** Kum 33:1; Amu 13:6; Kut 4:14-16; 1Fal 13:1
[h]**2:28** Kut 28:1; 30:7; 1Sam 22:18; 23:6-9; 30:7; Law 7:35-36; 8:7-8
[i]**2:29** Kum 12:5; Mt 10:37
[j]**2:30** Kut 29:19; Za 50:23; 91:15; Mit 8; 17; Isa 53:3; Neh 3:6; Mal 2:9; Yer 18:10; 1Nya 15:2; Za 18:20; 91:14; Yn 5:44; 12:26; 1Pet 1:7; Hes 11:20
[k]**2:31** 1Sam 4:11-18; 22:16-20
[l]**2:32** 1Sam 4:3; 22:17-20; Yer 7:12-14; 1Fal 2:26-27; Zek 8:4
[m]**2:33** Yer 29:32; Mal 2:12
[n]**2:34** Kum 13:4; 1Sam 4:11; 1Fal 13:3

moja. 35 [a]Mimi mwenyewe nitajiinulia kuhani mwaminifu, ambaye atafanya sawasawa na kile kilichoko moyoni mwangu na akilini mwangu. Nitaifanya nyumba yake kuwa imara, naye atahudumu mbele ya mpakwa mafuta wangu daima. 36 [b]Kisha kila mmoja aliyeachwa katika mbari yenu atakuja na kusujudu mbele yake kwa ajili ya kipande cha fedha na ganda la mkate akisema, “Niteue katika baadhi ya ofisi ya ukuhani ili niweze kupata chakula.” ’ ”

### *Bwana Amwita Samweli*

3 [c]Kijana Samweli alihudumu mbele za Bwana chini ya Eli. Katika siku zile neno la Mungu lilikuwa adimu, hapakuwepo na maono mengi.

2 [d]Usiku mmoja Eli, ambaye macho yake yalikuwa yamefifia sana kiasi kwamba aliona kwa shida sana, alikuwa amelala mahali pake pa kawaida. 3 [e]Taa ya Mungu bado ilikuwa haijazimika, na Samweli alikuwa amelala Hekaluni[f] mwa Bwana, ambapo Sanduku la Mungu lilikuwako. 4 [g]Kisha Bwana akamwita Samweli.

Samweli akajibu, “Mimi hapa.” 5 Naye akakimbia kwa Eli na kumwambia, “Mimi hapa, kwa kuwa umeniita.”

Lakini Eli akasema, “Sikukuita; rudi ukalale.” Hivyo akaenda kulala.

6 Bwana akaita tena, “Samweli!” Naye Samweli akaamka, kwenda kwa Eli na kusema, “Mimi hapa, kwa kuwa umeniita.”

Eli akasema, “Mwanangu, sikukuita, rudi ukalale.”

7 [h]Wakati huu Samweli alikuwa bado hajamjua Bwana. Neno la Bwana lilikuwa bado halijafunuliwa kwake.

8 Bwana akamwita Samweli mara ya tatu, naye Samweli akaamka kwenda kwa Eli na kusema, “Mimi hapa, kwa kuwa umeniita.”

Ndipo Eli akatambua kuwa Bwana alikuwa akimwita kijana. 9 Hivyo Eli akamwambia Samweli, “Nenda ukalale, na kama akikuita, sema, ‘Nena Bwana, kwa kuwa mtumishi wako anasikiliza.’ ” Hivyo Samweli akaenda na kulala mahali pake.

10 [i]Bwana akaja akasimama hapo, akiita kama mara zile nyingine, “Samweli! Samweli!”

Kisha Samweli akasema, “Nena Bwana, kwa kuwa mtumishi wako anasikiliza.”

11 [j]Naye Bwana akamwambia Samweli: “Tazama, nipo karibu kufanya kitu katika Israeli ambacho kitafanya masikio ya kila mmoja atakayesikia yawashe. 12 [k]Wakati huo nitatimiza dhidi ya Eli kila kitu nilichonena dhidi ya jamaa yake, kuanzia mwanzo mpaka mwisho. 13 [l]Kwa kuwa nilimwambia kwamba ningehukumu jamaa yake milele kwa sababu ya dhambi aliyoijua, wanawe kumkufuru Mungu, naye akashindwa kuwazuia. 14 [m]Kwa hiyo, nikaapa kuhusu nyumba ya Eli, ‘Hatia ya nyumba ya Eli kamwe haitaweza kufidiwa kwa dhabihu au sadaka.’ ”

15 [n]Samweli akalala mpaka asubuhi, kisha akafungua milango ya nyumba ya Bwana. Aliogopa kumwambia Eli yale maono, 16 lakini Eli akamwita na kumwambia, “Samweli mwanangu.”

Samweli akamjibu, “Mimi hapa.”

17 [o]Eli akamuuliza, “Ni nini alichokuambia? Usinifiche. Bwana na ashughulike nawe, tena kwa ukali, kama utanificha chochote

---

[a]**2:35** 1Nya 16:39; 29:22; 2Sam 8:17; 20:25; 1Fal 2:35; 4:4; Eze 44:15-16; 1Sam 10:1; 16:13; 2Sam 2:4; 12:7; 23:1; 1Fal 1:34; Za 89:20
[b]**2:36** Eze 44:10-14; 1Sam 3:12; 1Fal 2:27
[c]**3:1** 1Sam 2:11; Za 74:9; Mao 2:9; Eze 7:26; Amo 8:11
[d]**3:2** 1Sam 4:15; Mwa 27:1
[e]**3:3** Kut 25:31-38; Law 24:1-4; 1Sam 1:9; Kum 10:1-5; 1Fal 6:19; 8:1
[f]3 Hekaluni maana yake ndani ya Maskani ya Bwana.
[g]**3:4** Mwa 22:1; Kut 3:4
[h]**3:7** 1Sam 2:12; Hes 12:6; Mdo 19:2; Amo 3:7
[i]**3:10** Kut 3:4; Za 85:8; Mdo 9:6
[j]**3:11** 2Fal 21:12; Ay 15:21; Yer 19:3
[k]**3:12** 1Sam 2:27-36
[l]**3:13** 1Fal 1:6; 1Sam 2:12
[m]**3:14** 1Sam 2:25; Law 15:30-31; Isa 22:14; Hes 12:6; Yer 7:16; Ebr 10:26-31
[n]**3:15** 1Sam 3:2
[o]**3:17** 1Fal 22:14; Yer 23:28; 38:14; 42:4; Rut 1:17; 1:17; Mt 26:63

alichokuambia.” 18 [a]Kwa hiyo Samweli
akamwambia kila kitu, bila kumficha
chochote. Ndipo Eli akasema, “Yeye ni
BWANA; na afanye lile lililo jema machoni
pake!”
19 [b]BWANA alikuwa pamoja na Samweli
alipokuwa akikua, na hakuacha hata moja
ya maneno yake lianguke chini. 20 [c]Nao
Israeli wote kuanzia Dani hadi Beer-Sheba
wakatambua kuwa Samweli amethibitishwa
kuwa nabii wa BWANA. 21 [d]BWANA
akaendelea kutokea huko Shilo, na huko
kujidhihirisha kwa Samweli kwa njia ya
neno lake.

4 [e]Nalo neno la Samweli likaja kwa Israeli
yote.

*Wafilisti Wateka Sanduku La Mungu*

Basi Waisraeli walitoka kwenda kupigana
dhidi ya Wafilisti. Waisraeli wakapiga kambi
huko Ebenezeri, nao Wafilisti wakapiga
kambi huko Afeki. 2 Wafilisti wakapanga
safu za majeshi yao kupambana na Israeli,
wakati vita vilipoenea, Israeli wakashindwa
na Wafilisti, ambao waliwaua askari wa
Israeli wapatao 4,000 kwenye uwanja
wa vita. 3 [f]Askari waliporudi kambini,
wazee wa Israeli wakawauliza, “Kwa nini
BWANA ameruhusu leo tushindwe mbele
ya Wafilisti? Tuleteni Sanduku la Agano
la BWANA kutoka Shilo, ili lipate kwenda
pamoja nasi, na kutuokoa kutoka mikono
ya adui zetu.”
4 [g]Hivyo wakawatuma watu huko
Shilo, nao wakalichukua Sanduku la
Agano la BWANA Mwenye Nguvu Zote,
aliyekaa kwenye kiti chake cha enzi kati
ya makerubi. Nao wale wana wawili wa
Eli, Hofni na Finehasi, walikuwako huko
pamoja na Sanduku la Agano la Mungu.
5 [h]Wakati Sanduku la Agano la BWANA
lilikuja kambini, Waisraeli wote wakapiga
kelele kwa sauti kuu hata ardhi ikatikisika.
6 [i]Wafilisti waliposikia makelele wakauliza,
“Ni nini makelele haya yote katika kambi
ya Waebrania?”

Walipofahamu kuwa Sanduku la BWANA
limekuja kambini, 7 [j]Wafilisti wakaogopa,
wakasema, “Mungu amekuja kambini, ole
wetu. Halijatokea jambo kama hili tangu
hapo. 8 [k]Ole wetu! Ni nani atakayetuokoa
kutoka mikononi mwa miungu hii yenye
nguvu? Ni miungu ile iliyowapiga Wamisri
kwa mapigo ya aina zote huko jangwani.
9 [l]Tuweni hodari, enyi Wafilisti! Tuweni
wanaume, la sivyo mtakuwa watumwa wa
Waebrania, kama wao walivyokuwa kwenu.
Kuweni wanaume, mpigane!”
10 [m]Basi Wafilisti wakapigana, nao
Waisraeli wakashindwa na kila mtu
akakimbilia hemani mwake. Mauaji
yalikuwa makubwa sana, Israeli
wakapoteza askari 30,000 waendao kwa
miguu. 11 [n]Sanduku la Mungu likatekwa, na
hao wana wawili wa Eli, Hofni na Finehasi,
wakauawa.

*Kifo Cha Eli*

12 [o]Siku ile ile mtu mmoja wa kabila
la Benyamini akakimbia kutoka kwenye
uwanja wa vita na kwenda Shilo, nguo zake
zikiwa zimeraruka na akiwa na mavumbi
kichwani mwake. 13 [p]Alipofika, Eli alikuwa
ameketi juu ya kiti chake kando ya barabara
akiangalia, kwa sababu moyo wake ulikuwa
na hofu kwa ajili ya Sanduku la Mungu.

---

[a]**3:18** Amu 10:15; 2:16; Mwa 18:25; 1Sam 16:10-12; Isa 39:8; 1Pet 5:6
[b]**3:19** Mwa 21:22; Hes 14:43; Amu 13:24; 1Sam 9:6; Mwa 39:2
[c]**3:20** Amu 20:1; Kum 18:22; Eze 33:33; Amu 20:1
[d]**3:21** Mwa 12:7; Hes 12:6; Amo 3:7
[e]**4:1** 1Sam 5:1; 7:12; 29:1; Yos 12:18; 1Fal 20:26
[f]**4:3** Yos 6:7; 7:7; 18:1; 1Sam 2:32; 2Nya 13:8
[g]**4:4** Mwa 3:24; Kut 25:23; 2Sam 6:2; Za 80:1; Hes 7:89
[h]**4:5** Yos 6:5-10
[i]**4:6** Mwa 14:13
[j]**4:7** Kut 15:14
[k]**4:8** Kut 12:30; 1Sam 5:12; Ufu 11:6
[l]**4:9** Amu 13:1; 1Kor 16:13; 2Sam 10:12; 1Nya 19:13
[m]**4:10** 2Sam 18:17; 2Fal 14:12; Kum 28:25; Law 26:17
[n]**4:11** Za 78:64; Yer 7:12; 1Sam 2:32
[o]**4:12** Eze 24:26; 33:21; Yos 7:6; Neh 9:1; 2Sam 1:2; Ay 2:12
[p]**4:13** 1Sam 1:9

Mtu yule alipoingia mjini na kueleza
kilichokuwa kimetokea, mji wote ukalia.
14 Eli akasikia kelele za kilio, naye
akauliza, “Ni nini maana ya makelele
haya?”
Yule mtu akafanya haraka kwenda
kwa Eli, 15 wakati huu Eli alikuwa na
miaka tisini na minane nayo macho yake
yalikuwa yamepofuka na hakuweza kuona.
16 [a]Akamwambia Eli, “Mimi nimetoka vitani
sasa hivi, nimekimbia kutoka huko leo hii.”
Eli akamuuliza, “Je, mwanangu, ni nini
kimetokea huko?”
17 [b]Yule mtu aliyeleta habari akajibu,
“Israeli amekimbia mbele ya Wafilisti,
nalo jeshi limepata hasara kubwa. Pia wana
wako wawili, Hofni na Finehasi, wamekufa,
na Sanduku la Mungu limetekwa.”
18 [c]Mara alipotaja Sanduku la Mungu,
Eli alianguka kutoka kwenye kiti chake
kwa nyuma kando ya lango. Shingo yake
ikavunjika naye akafa, kwa kuwa alikuwa
mzee tena mzito. Alikuwa amewaongoza
Israeli kwa miaka arobaini.
19 Mkwewe, mke wa Finehasi, alikuwa
mjamzito na karibu wakati wa kujifungua.
Aliposikia habari kwamba Sanduku la
Mungu limetekwa na ya kuwa baba mkwe
wake na mumewe wamekufa, akapata
utungu naye akajifungua lakini akazidiwa
na utungu. 20 [d]Alipokuwa akifa, wanawake
waliokuwa wanamhudumia wakamwambia,
“Usikate tamaa, umemzaa mwana.” Lakini
hakujibu wala kuweka maanani.
21 [e]Alimwita yule mtoto Ikabodi,[f] akisema,
“Utukufu umeondoka katika Israeli,” kwa
sababu ya kutekwa kwa Sanduku la Mungu
na vifo vya baba mkwe na mumewe.
22 [g]Akasema, “Utukufu umeondoka katika
Israeli, kwa kuwa Sanduku la Mungu
limetekwa.”

*Sanduku La Agano Huko Ashdodi Na Ekroni*

5 [h]Baada ya Wafilisti kuteka Sanduku la
Mungu, walilichukua kutoka Ebenezeri
mpaka Ashdodi. 2 [i]Kisha wakaliingiza lile
Sanduku ndani ya hekalu la Dagoni na
kuliweka kando ya huyo Dagoni. 3 [j]Watu wa
Ashdodi walipoamka asubuhi na mapema
kesho yake, kumbe, wakamkuta Dagoni
ameanguka chini kifudifudi mbele ya
Sanduku la BWANA! Wakamwinua Dagoni na
kumrudisha mahali pake. 4 [k]Lakini asubuhi
iliyofuata, walipoamka kumbe, walimkuta
huyo Dagoni ameanguka chini kifudifudi
mbele ya Sanduku la BWANA! Kichwa chake
na mikono vilikuwa vimevunjwa navyo
vimelala kizingitini, ni kiwiliwili chake
tu kilichokuwa kimebaki. 5 [l]Ndiyo sababu
mpaka leo makuhani wa Dagoni wala
wengine waingiao katika hekalu la Dagoni
huko Ashdodi hawakanyagi kizingiti.
6 [m]Mkono wa BWANA ulikuwa mzito
juu ya watu wa Ashdodi na vijiji jirani,
akaleta uharibifu juu yao na kuwatesa
kwa majipu. 7 Watu wa Ashdodi walipoona
kile kilichokuwa kikitokea, wakasema,
“Sanduku la Mungu wa Israeli kamwe
lisikae hapa pamoja na sisi, kwa sababu
mkono wake ni mzito juu yetu na juu ya
Dagoni mungu wetu.” 8 [n]Basi wakawaita
watawala wote wa Wafilisti pamoja na
kuwauliza, “Tutafanya nini na hili Sanduku
la Mungu wa Israeli?”
Wakajibu, “Sanduku la Mungu wa Israeli
na liende Gathi.” Basi wakalihamisha
Sanduku la Mungu wa Israeli.
9 [o]Lakini baada ya kulihamisha, mkono
wa BWANA ulikuwa dhidi ya huo mji wa
Gathi, akiuweka katika fadhaa kuu. Mungu
akawatesa watu wa huo mji, vijana kwa

---

[a]**4:16** 2Sam 1:4
[b]**4:17** 1Sam 22:18; Za 78:64; 78:61
[c]**4:18** Amu 2:16; 16:31; 1Sam 2:31
[d]**4:20** Mwa 35:17
[e]**4:21** Mwa 35:18; Kut 24:16; Za 106:26; Yer 2:11; Eze 1:28; 9:3; 10:18
[f]21 Ikabodi maana yake Utukufu wa BWANA umeondoka.
[g]**4:22** Kut 24:16; Za 78:61; Yer 7:12

[h]**5:1** 1Sam 4:1; Yos 11:22; 13:3; 1Sam 7:12
[i]**5:2** Amu 16:23; Isa 2:18; 19:1; 46:1
[j]**5:3** Isa 40:20; 41:7; Yer 10:4; Isa 46:7; Kut 12:12; 18:11; 1Nya 16:24-26; Za 95:3; 97:9; Isa 19:1; 46:1, 2, 7; Nah 1:14
[k]**5:4** Eze 6:6; Mik 1:7; Isa 40:18; Yer 50:2
[l]**5:5** Sef 1:9
[m]**5:6** Za 32:4; 78:66; Mdo 13:11; 2Sam 6:7; Kum 28:27; 1Sam 6:5
[n]**5:8** Amu 16:18; Yos 11:12
[o]**5:9** Kut 14:24; Kum 2:15

wazee, kwa kuwaletea majipu. 10 [a]Basi wakapeleka Sanduku la Mungu Ekroni.

Wakati Sanduku la Mungu lilipokuwa linaingia Ekroni, watu wa Ekroni walilia wakisema “Wamelileta Sanduku la Mungu wa Israeli kwetu ili kutuua sisi na watu wetu.” 11 Basi wakawaita watawala wote wa Wafilisti pamoja na kusema, “Liondoeni Sanduku la Mungu wa Israeli na lirudishwe mahali pake, la sivyo litatuua sisi na watu wetu.” Kwa kuwa kifo kilikuwa kimeujaza mji hofu; kwani mkono wa Mungu ulikuwa mzito sana juu yake. 12 [b]Wale ambao hawakufa walipatwa na majipu, na kilio cha mji kilikwenda juu hadi mbinguni.

### *Sanduku La Mungu Larudishwa Israeli*

6 Sanduku la BWANA lilipokuwa limekaa katika nchi ya Wafilisti kwa miezi saba, 2 [c]Wafilisti waliwaita makuhani wa Dagoni na waaguzi, na kuwaambia, “Tutafanya nini na hili Sanduku la BWANA? Tuambieni jinsi tutakavyolirudisha mahali pake.”

3 [d]Wakajibu, “Kama mtalirudisha Sanduku la Mungu wa Israeli, msilirudishe mikono mitupu bali kwa vyovyote mpelekeeni sadaka ya hatia. Kisha mtaponywa, nanyi mtafahamu kwa nini mkono wake haujaondolewa kwenu.”

4 [e]Wafilisti wakawauliza, “Ni sadaka gani ya hatia tutakayompelekea?”

Wakajibu, “Majipu matano ya dhahabu na panya wa dhahabu watano, kulingana na idadi ya watawala wa Wafilisti, kwa sababu tauni iyo hiyo imewaua ninyi na watawala wenu. 5 [f]Tengenezeni mifano ya majipu na ya panya wale wanaoharibu nchi yenu, nanyi mheshimuni Mungu wa Israeli. Labda ataondoa mkono wake kutoka kwenu na kwa miungu yenu na nchi yenu. 6 [g]Kwa nini ninyi mnafanya mioyo yenu migumu kama Wamisri na Farao walivyofanya? Je, alipowatendea kwa ukali, hawakuwaachia Waisraeli wakaenda zao?

7 [h]“Sasa basi, wekeni gari jipya la kukokotwa pamoja na ng’ombe wawili ambao wamezaa lakini ambao kamwe hawajafungwa nira. Fungieni hao ng’ombe hilo gari, lakini ondoeni ndama wao na mwaweke zizini. 8 Chukueni hilo Sanduku la BWANA na mliweke juu ya gari la kukokotwa, na ndani ya kasha kando yake wekeni hivyo vitu vya dhahabu mnavyompelekea BWANA kama sadaka ya hatia. Lipelekeni, 9 [i]lakini liangalieni kwa makini. Iwapo litakwenda katika nchi yake lenyewe, kuelekea Beth-Shemeshi, basi tutajua kwamba BWANA ndiye alileta haya maafa makubwa juu yetu. Lakini kama halikwenda, basi tutajua kwamba haukuwa mkono wa BWANA uliotupiga na kwamba iliyotokea kwetu ni ajali.”

10 Basi wakafanya hivyo. Wakachukua ng’ombe wawili wa aina hiyo, wakawafungia hilo gari la kukokotwa, nao ndama wao wakawekwa zizini. 11 Wakaliweka Sanduku la BWANA juu ya hilo gari la kukokotwa pamoja na lile kasha lenye ile mifano ya panya wa dhahabu na ya majipu ya dhahabu. 12 Kisha hao ng’ombe wakaenda moja kwa moja kuelekea Beth-Shemeshi, wakishuka bila kugeuka kuume au kushoto, huku wakilia njia yote. Watawala wa Wafilisti waliwafuata hao ng’ombe hadi mpakani mwa Beth-Shemeshi.

13 [j]Wakati huu watu wa Beth-Shemeshi walikuwa wakivuna ngano yao huko bondeni, walipoinua macho yao na kuona lile Sanduku, wakafurahi kuliona. 14 [k]Lile gari la kukokotwa lilikuja mpaka kwenye shamba la Yoshua wa Beth-Shemeshi, nalo likasimama kando ya mwamba mkubwa. Watu wakapasua mbao za lile gari la

---

[a]**5:10** Yos 13:3
[b]**5:12** 1Sam 4:8; Kut 11:6; Mit 21:13; Isa 15:3; Yer 25:34; Amo 5:17; Yak 2:13
[c]**6:2** Kut 7:11; Isa 44:25; Mwa 41:8; Dan 2:2; 5:7; Mit 2:4
[d]**6:3** Kut 22:29; 34:20; Law 5; 15; Kum 16:16
[e]**6:4** Yos 13:3; Amu 3:3; 2Sam 24:25
[f]**6:5** 1Sam 5:6; Yos 7:19; Ufu 14:7; Isa 42:12; Yn 9:24; 1Nya 16:28; Mal 2:2; Kut 9:3; Za 39:10; Mdo 13:11
[g]**6:6** Kut 4:21; 10:2; 12:33; 7:13; 9:34; Za 105:38
[h]**6:7** 2Sam 6:3; 1Nya 13:7; Hes 19:2
[i]**6:9** Yos 15:10; 21:16
[j]**6:13** Mwa 30:14; Rut 2:23; 1Sam 12:17
[k]**6:14** 1Sam 11:7; 2Sam 24:22; 1Fal 9:21

kukokotwa na kutoa dhabihu wale ng'ombe
kama sadaka ya kuteketezwa kwa BWANA.
15 [a]Walawi walilishusha Sanduku la BWANA,
pamoja na lile kasha lililokuwa na vile
vitu vya dhahabu na kuviweka juu ya ule
mwamba mkubwa. Siku ile watu wa Beth-
Shemeshi wakatoa sadaka za kuteketezwa
na dhabihu kwa BWANA. 16 [b]Wale watawala
watano wa Wafilisti waliona haya yote, nao
wakarudi siku ile ile mpaka Ekroni.

17 [c]Haya ndiyo yale majipu ya dhahabu
Wafilisti waliyotuma kama sadaka ya hatia
kwa BWANA, moja kwa ajili ya Ashdodi,
moja kwa Gaza, moja kwa Ashkeloni, moja
kwa Gathi, na moja kwa Ekroni. 18 Nayo
hesabu ya wale panya wa dhahabu ilikuwa
kulingana na idadi ya miji ya Wafilisti ya
watawala watano wa Wafilisti: miji yao
iliyozungukwa na maboma, pamoja na
vijiji vya miji hiyo. Ule mwamba mkubwa,
ambao juu yake waliliweka lile Sanduku la
BWANA, ni ushahidi hadi leo katika shamba
la Yoshua wa Beth-Shemeshi.

19 [d]Lakini Mungu aliwapiga baadhi ya
watu wa Beth-Shemeshi, akiwaua watu
sabini miongoni mwao kwa sababu
walichungulia ndani ya Sanduku la BWANA.
Watu wakaomboleza kwa sababu ya pigo
zito kutoka kwa BWANA, 20 [e]nao watu wa
Beth-Shemeshi wakauliza, "Ni nani awezaye
kusimama mbele za BWANA, huyu Mungu
aliye mtakatifu? Sanduku litapanda kwenda
kwa nani kutoka hapa?"

21 [f]Kisha wakatuma wajumbe kwa watu
wa Kiriath-Yearimu, wakisema, "Wafilisti
wamerudisha Sanduku la BWANA. Shukeni
na mlipandishe huko kwenu."

7 [g]Kisha watu wa Kiriath-Yearimu wakaja
na kulichukua Sanduku la BWANA.
Wakalipeleka katika nyumba ya Abinadabu
juu kilimani na kumweka Eleazari mwanawe
wakfu kulichunga Sanduku la BWANA.

*Samweli Awatiisha Wafilisti Huko Mispa*

2 [h]Sanduku la BWANA lilibakia huko
Kiriath-Yearimu kwa muda mrefu, yaani
jumla ya miaka ishirini, nao watu wa
Israeli wakaomboleza na kumtafuta
BWANA. 3 [i]Naye Samweli akawaambia
nyumba yote ya Israeli, "Ikiwa mtamrudia
BWANA kwa mioyo yenu yote, basi iacheni
miungu migeni na Maashtorethi na kujitoa
wenyewe kwa BWANA na kumtumikia yeye
peke yake, naye atawaokoa ninyi na mkono
wa Wafilisti." 4 Hivyo Waisraeli wakaweka
mbali Mabaali yao na Maashtorethi, nao
wakamtumikia BWANA peke yake.

5 [j]Kisha Samweli akasema, "Wakusanyeni
Israeli wote huko Mispa, nami nitawaombea
ninyi kwa BWANA." 6 [k]Walipokwisha
kukutanika huko Mispa, walichota maji na
kuyamimina mbele za BWANA. Siku hiyo
walifunga na wakaungama, wakisema,
"Tumetenda dhambi dhidi ya BWANA."
Naye Samweli alikuwa kiongozi[l] wa Israeli
huko Mispa.

7 [m]Wafilisti waliposikia kwamba Israeli
wamekusanyika huko Mispa, watawala wa
Wafilisti wakapanda ili kuwashambulia.
Waisraeli waliposikia habari hiyo,
waliogopa kwa sababu ya Wafilisti.
8 [n]Wakamwambia Samweli, "Usiache
kumlilia BWANA, Mungu wetu, kwa ajili
yetu, ili apate kutuokoa na mikono ya

---

[a]**6:15** Yos 3:3; 21:16
[b]**6:16** Yos 13:3; Amu 16:23; 1Sam 29:2
[c]**6:17** Yos 13:3
[d]**6:19** 2Sam 6:7; Kut 19:21; Hes 4:5; Law 10:1-3; 2Sam 6:7; Kol 2:8; 1Pet 4:17
[e]**6:20** 2Sam 6:9; Za 130:3; Ufu 6:17; Mal 3:2; Law 11:45
[f]**6:21** Yos 9:17; 15:9, 60; 1Nya 13:5-6; Amu 18:12
[g]**7:1** Yos 6:7; 2Sam 6:3; 1Nya 13:7; 1Sam 6:21; Za 132:6
[h]**7:2** 1Nya 13:5; Za 132:6; 1Nya 13:3
[i]**7:3** Kut 30:10; 2Fal 18:5; 23:25; Yer 24:7; Mwa 31:19; Amu 2:12-13; 1Sam 12:10; 31:10; Yoe 2:12; Yos 24:14; Kum 6; 13; Mt 4:10; Lk 4:8; Amu 2:18
[j]**7:5** 1Sam 1:20; Za 99:6; Yer 15:1; Yos 11:3; Amu 21:5; 1Sam 10:17; Mwa 20:7; Kum 9:19
[k]**7:6** Yos 11:3; Mao 2:19; Amu 2:16; 16:31; Neh 9:1, 2; 2Sam 14:14; Dan 9:3; Yoe 2:12; Law 26:40; Amu 10:10; 1Fal 8:47; Ay 33:27, 28; Za 106:6
[l]6 Kiongozi hapa maana yake mwamuzi.
[m]**7:7** 1Sam 17:11
[n]**7:8** Kut 32:30; Hes 21:7; 1Sam 12:19, 23; 1Fal 18:24; Isa 37:4; Yer 15:1; 27:18

Wafilisti.” 9 [a]Kisha Samweli akamchukua mwana-kondoo anyonyaye na kumtoa mzima kama sadaka ya kuteketezwa kwa BWANA. Akamlilia BWANA kwa niaba ya Israeli, naye BWANA akamjibu.

10 [b]Samweli alipokuwa anatoa hiyo dhabihu ya kuteketezwa, Wafilisti wakasogea karibu ili kupigana vita na Israeli. Lakini siku ile BWANA alinguruma kwa ngurumo kubwa dhidi ya Wafilisti na kuwafanya wafadhaike na kutetemeka hivi kwamba walikimbizwa mbele ya Waisraeli. 11 Watu wa Israeli wakatoka mbio huko Mispa na kuwafuatia Wafilisti, wakiwachinja njiani hadi mahali chini ya Beth-Kari.

12 [c]Ndipo Samweli akachukua jiwe na kulisimamisha kati ya Mispa na Sheni. Akaliita Ebenezeri,[d] akisema, “Hata sasa BWANA ametusaidia.” 13 [e]Basi Wafilisti wakashindwa na hawakuvamia nchi ya Israeli tena.

Katika maisha yote ya Samweli, mkono wa BWANA ulikuwa dhidi ya Wafilisti. 14 [f]Miji kuanzia Ekroni hadi Gathi, ile ambayo Wafilisti walikuwa wameiteka kutoka Israeli, ilirudishwa kwake, naye Israeli akazikomboa nchi jirani mikononi mwa Wafilisti. Kukawepo amani kati ya Israeli na Waamori.

15 [g]Samweli akaendelea kama mwamuzi juu ya Israeli siku zote za maisha yake. 16 [h]Mwaka hadi mwaka aliendelea kuzunguka kutoka Betheli mpaka Gilgali na Mispa, akiamua Israeli katika sehemu hizo zote. 17 [i]Lakini kila mara alirudi Rama, kulikokuwa nyumbani kwake, huko pia aliwaamua Israeli. Naye huko alimjengea BWANA madhabahu.

*Israeli Waomba Mfalme*

8 [j]Samweli alipokuwa mzee, akaweka wanawe kuwa waamuzi wa Israeli. 2 [k]Mzaliwa wa kwanza alikuwa Yoeli, na la wa pili lilikuwa Abiya, nao wakatumika huko Beer-Sheba. 3 [l]Lakini wanawe hawakuenenda katika njia zake. Waliziacha wakageukia faida za udanganyifu nao wakapokea rushwa na kupotosha haki.

4 [m]Basi wazee wote wa Israeli wakakusanyika pamoja na kumjia Samweli huko Rama. 5 [n]Wakamwambia, “Wewe umekuwa mzee, nao wanao hawaenendi katika njia zako, sasa tuteulie mfalme wa kutuongoza, kama ilivyo kwa mataifa mengine yote.”

6 [o]Lakini wao waliposema, “Tupe mfalme wa kutuongoza,” hili lilimchukiza Samweli, hivyo akamwomba BWANA. 7 [p]Naye BWANA akamwambia: “Sikiliza yale yote watu wanakuambia. Si wewe ambaye wamekukataa, bali wamenikataa mimi kuwa mfalme wao. 8 [q]Kama vile walivyofanya tangu siku nilipowapandisha kutoka Misri mpaka siku hii ya leo; wakiniacha mimi na kutumikia miungu mingine, ndivyo wanavyokufanyia wewe. 9 [r]Sasa wasikilize, lakini waonye kwa makini na uwafahamishe yale watakayotendewa na mfalme atakayewatawala.”

10 [s]Samweli akawaambia wale watu waliokuwa wakiomba wapewe mfalme

---

[a]**7:9** Za 99:6; Kut 32:11; Kum 19:9; Yer 15:1
[b]**7:10** Kut 9:23; 14:24; 1Sam 2:10; Mwa 35:5; 2Sam 22:14-15; Yos 10:10
[c]**7:12** Mwa 28:22; Kum 27:2; Yos 4:9; 1Sam 4; 1
[d]12 Ebenezeri maana yake jiwe la usaidizi.
[e]**7:13** Amu 13:5; 1Sam 13:5
[f]**7:14** Yos 13:3; Amu 1:34
[g]**7:15** 1Sam 12:11; Amu 2:16-18
[h]**7:16** Mwa 12:8; Yos 10:43; 1Sam 10:8; Amo 5:5; Mdo 13; 20
[i]**7:17** Yos 18:25; 1Sam 8:4; 15:34; 19:18; 25:1; 28:3; 9:12; 14:35; 20:6; 2Sam 24:25
[j]**8:1** Kum 16:18-19; Amu 10:4; 12:14
[k]**8:2** 1Nya 6:28; Mwa 22; 19; 1Fal 19:3; Amo 5:4-5
[l]**8:3** 1Sam 2:12; Neh 9:29; Ay 34:27; Za 14:3; 58:3; Isa 53:6; Kut 23:8; 1Sam 12:3; Mit 17:23; Kut 23:2; Kum 16:19
[m]**8:4** Amu 11:11; 1Sam 11:3; 7:17
[n]**8:5** Kum 17:14-20; 1Sam 10:19; 12:12-13; 3:20; 12:2; Hos 13:11
[o]**8:6** Hos 13:10; 1Sam 12:17; 15:11; 16:1
[p]**8:7** 1Sam 12:1; Hes 11:20; Kut 16:8; Mt 10:24-25; Lk 10:16; Yn 13:16; 1Sam 10:19
[q]**8:8** 1Sam 12:10; 2Fal 21:22; Yer 2:17
[r]**8:9** Kum 17:14-20; 1Sam 8:11-18; 10:25
[s]**8:10** Kut 19:7

maneno yote ya Bwana. 11 [a]Akasema,
“Hivi ndivyo atakavyowatendea mfalme
atakayewatawala. Atawachukua wana
wenu na kuwafanya watumike kwa magari
yake ya vita na farasi, nao watakimbia
mbele ya magari yake. 12 [b]Baadhi yao
atawaweka kuwa majemadari wa jeshi
wa maelfu na majemadari wa jeshi wa
hamsini, wengine kulima mashamba yake
na kuvuna mavuno yake, pia na wengine
kutengeneza silaha za vita na vifaa kwa ajili
ya magari yake. 13 Atawachukua binti zenu
kuwa watengeneza manukato, wapishi na
waokaji. 14 [c]Atayachukua mashamba yenu
yaliyo mazuri, mashamba ya mizabibu na
mashamba yenu ya mizeituni na kuwapa
watumishi wake. 15 [d]Ataichukua sehemu ya
kumi ya nafaka yenu na ya zabibu zenu
na kuwapa maafisa wake na watumishi
wake. 16 Atawachukua watumishi wenu wa
kiume na wa kike, na ng’ombe wenu walio
wazuri sana na punda kwa matumizi yake
mwenyewe. 17 Atachukua sehemu ya kumi
ya makundi yenu ya kondoo na mbuzi,
na ninyi wenyewe mtakuwa watumwa
wake. 18 [e]Siku ile itakapowadia, mtalia
kwa kutaka msaada kutokana na mfalme
mliyemchagua, naye Bwana hatawajibu.”

19 [f]Lakini watu wakakataa kumsikiliza
Samweli wakasema, “Hapana! Tunataka
mfalme wa kututawala. 20 Kisha tutakuwa
kama mataifa mengine yote, tukiwa na
mfalme wa kutuongoza na kwenda mbele
yetu na kutupigania vita vyetu.”

21 [g]Samweli aliposikia yote watu
waliyosema, akarudia kuyasema mbele za
Bwana. 22 [h]Bwana akamjibu, “Wasikilize
na uwape mfalme.”

Kisha Samweli akawaambia watu wa
Israeli, “Kila mmoja arudi mjini kwake.”

### *Samweli Anamtia Sauli Mafuta*

9 [i]Kulikuwako Mbenyamini mmoja, mtu
maarufu, ambaye aliitwa Kishi mwana
wa Abieli, mwana wa Serori, mwana wa
Bekorathi, mwana wa Afia wa Benyamini.
2 [j]Alikuwa na mwana aliyeitwa Sauli, kijana
anayevutia sana, hakuwepo aliyelingana
naye miongoni mwa Waisraeli, alikuwa
mrefu kuliko wengine wote.

3 [k]Basi punda wa Kishi baba yake Sauli
walipotea, naye Kishi akamwambia
mwanawe Sauli, “Mchukue mmoja
wa watumishi mwende pamoja naye
kuwatafuta punda.” 4 [l]Hivyo akapita
katika nchi ya vilima ya Efraimu na katika
eneo la Shalisha, lakini hawakuwapata.
Wakaendelea katika sehemu ya Shaalimu,
lakini punda hawakuwepo huko. Kisha
wakapita katika nchi ya Benyamini, lakini
hawakuwapata.

5 [m]Walipofika sehemu ya Sufu, Sauli
akamwambia mtumishi aliyekuwa pamoja
naye, “Njoo, sisi na turudi, au baba yangu
ataacha kufikiria juu ya punda na kuanza
kufadhaika kutuhusu sisi.”

6 [n]Lakini mtumishi akajibu, “Tazama,
katika mji huu yupo mtu wa Mungu,
anayeheshimiwa sana na kila kitu asemacho
hutokea kweli. Sasa na twende huko.
Huenda atatuambia twende njia ipi.”

7 [o]Sauli akamwambia mtumishi wake,
“Kama tukienda, tutampa nini huyo mtu?

---

[a]**8:11** 1Sam 10:25; 14:52; Mwa 41:46; Kum 17:16; 2Sam 15:1; 2Nya 1:14; 9:25; Wim 3:7; 1Nya 1:5
[b]**8:12** Kum 1:15; 1Sam 22:7
[c]**8:14** 1Sam 28:6; Ay 27:9; 35:12-13; Za 18:41; 66:18; Mit 1:28; Isa 58:4; 59:2; Yer 14:12; Eze 8:18; Mik 3:4; 1Sam 10:25; 1Fal 12:4
[d]**8:15** Mwa 41:34; 1Sam 17:25
[e]**8:18** 1Sam 28:6; Ay 27:9; 35:12-13; Za 18:41; 66:18; Mit 1:28; Isa 58:4; 59:2; Yer 14:12; Eze 8:18; Mik 3:4; 1Sam 10:25; 1Fal 12:4
[f]**8:19** Mit 1:24; Isa 50:2; 66:4; Yer 7:13; 8; 12; 13; 10; 44:16; Mdo 13:21
[g]**8:21** Amu 11:11
[h]**8:22** Hos 13:11
[i]**9:1** Yos 18:11-20; Rut 2:1; 1Sam 14:51; 1Nya 8:33; 9:39; Es 2:5; Mdo 13:21
[j]**9:2** Mwa 39:6; 1Sam 10:23-24
[k]**9:3** 1Sam 10:14-16
[l]**9:4** Yos 24:33; 2Fal 4:42; 1Sam 10:2
[m]**9:5** 1Sam 1:1; 10:1
[n]**9:6** Kum 33:1; Amu 13:6; 1Sam 3:19; 1Fal 13:1; 2Fal 6:6; 1Tim 6:11; 1Sam 3:19; Isa 44:26; Mt 24:35
[o]**9:7** Mwa 32:20; 1Fal 13:7; 14:3; 2Fal 4:42; 5:5, 15; Yer 40:5; Amu 6:18; 13:17

Chakula kimekwisha kwenye mifuko yetu.
Hatuna zawadi ya kumpelekea huyo mtu
wa Mungu. Je tuna nini?”
8 Mtumishi akamjibu Sauli tena, akasema,
“Tazama, nina fedha robo shekeli.[a] Hiyo
nitampa huyo mtu wa Mungu ili aweze
kutuambia twende kwa njia ipi.” 9 [b](Zamani
katika Israeli, kama mtu alikwenda kuuliza
neno kwa Mungu, angalisema, “Njoo na
twende kwa mwonaji,” kwa sababu nabii
wa sasa alikuwa akiitwa mwonaji.)
10 Sauli akamwambia mtumishi wake,
“Vyema, njoo na twende.” Basi wakaenda
mjini alipokuwepo huyo mtu wa Mungu.
11 [c]Walipokuwa wakipanda mlima
kwenda mjini, wakakutana na baadhi ya
wasichana wanakuja kuchota maji, nao
wakawauliza, “Je, mwonaji yuko?”
12 [d]Wakajibu, “Yuko, yu mbele yenu
amewatangulia, sasa fanyeni haraka, ndiyo
tu amekuja mjini kwetu leo, kwa kuwa watu
wana dhabihu huko mahali pa juu. 13 [e]Mara
tu mwingiapo mjini, mtamkuta kabla
hajapanda kwenda mahali pa juu kula.
Watu hawataanza kula mpaka atakapofika
kwa sababu ni lazima kwanza yeye
abariki dhabihu, ndipo wale walioalikwa
watakapokula. Pandeni sasa, mtamkuta
kwa wakati huu.”
14 Wakapanda mjini, nao walipokuwa
wakiingia mjini, tazama, Samweli alikuwa
akija kuelekea walikokwenda mahali pa
juu.
15 [f]Basi siku moja kabla Sauli hajaja,
Bwana alikuwa amemfunulia Samweli
jambo hili: 16 [g]“Kesho wakati kama
huu nitakupelekea mtu kutoka nchi ya
Benyamini. Umtie mafuta awe kiongozi
juu ya watu wangu Israeli, ndiye
atakayewakomboa watu wangu na mkono
wa Wafilisti. Nimewaangalia watu wangu,
kwa kuwa kilio chao kimenifikia.”
17 [h]Samweli alipomwona Sauli,
Bwana akamwambia, “Huyu ndiye mtu
niliyekuambia habari zake, kwamba yeye
atawatawala watu wangu.”
18 Sauli akamkaribia Samweli langoni
na kumuuliza, “Tafadhali, je, waweza
kuniambia mahali nyumba ya mwonaji
ilipo?”
19 Samweli akamjibu Sauli, “Mimi ndiye
mwonaji, panda utangulie mbele yangu
mpaka mahali pa juu, kwa kuwa leo
itakupasa kula pamoja nami na asubuhi
nitakuruhusu uende na nitakuambia yale
yote yaliyo moyoni mwako. 20 [i]Kuhusu wale
punda uliowapoteza siku tatu zilizopita,
usifadhaike kwa habari yao; wamepatikana.
Ni kwa nani ambaye shauku yote ya Israeli
imeelekea, kama si kwako na jamaa yote
ya baba yako?”
21 [j]Sauli akajibu, “Je, mimi si Mbenyamini,
kutoka kabila dogo kuliko yote ya Israeli,
nao ukoo wangu si ndio mdogo kuliko koo
zote za kabila la Benyamini? Kwa nini
uniambie jambo la namna hiyo?”
22 Kisha Samweli akamleta Sauli
na mtumishi wake ndani ukumbini
na kuwaketisha mahali pa heshima
zaidi miongoni mwa wale waliokuwa
wamealikwa; jumla yao walikuwa kama
watu thelathini. 23 Samweli akamwambia
mpishi, “Leta ile sehemu ya nyama
niliyokupa, ile niliyokuambia iweke kando.”

---

[a]8 Robo shekeli ni sawa na gramu 3.
[b]**9:9** Mwa 25:22; 2Sam 15:27; 24:11; 17:13; 1Nya 9:22; 21:9; 26:28; 29:29; 2Nya 19:2; Isa 29:10; 30:10; Amo 7:12; Kut 28:30; Hes 27:21; Amu 1:1; 20:18-28; 2Sam 24:11; 2Fal 17:13
[c]**9:11** Mwa 24:11-13; Kut 2:16
[d]**9:12** Hes 28:11-15; 1Sam 7:17; Law 26:30; 1Fal 3:2
[e]**9:13** Mt 14:19; 1Kor 10:16; 1Tim 4:3-5
[f]**9:15** 1Sam 24:11; Za 25:14; Mk 11:2-4; Mdo 13:11
[g]**9:16** Kut 30:25; 1Sam 2:35; 12:3; 15:1; 26:9; 2Fal 11:12; Za 2:2; 2Sam 7:8; 1Fal 8; 16; 1Nya 5:2; Kut 3:8; 1Sam 23:4; 2Sam 3:18; Mwa 16:11; Za 102:1
[h]**9:17** 1Sam 16:12; Hos 13:11
[i]**9:20** 1Sam 12:13; Ezr 6:8; Isa 60:4-9; Dan 2:44; Hag 2:7; Mal 3:1
[j]**9:21** Za 68:27; Kut 3:11; Mt 2:6; 1Kor 15:9; Amu 6:15; 20:35, 46; 1Sam 18:18; 15:17

24 [a]Hivyo mpishi akachukua mguu pamoja
na kile kilichokuwa juu yake akaiweka
mbele ya Sauli. Samweli akasema, “Hiki
ndicho ambacho kimewekwa kwa ajili
yako. Ule, kwa sababu kilitengwa kwa
ajili yako kwa tukio hili, tangu niliposema,
‘Nimewaalika wageni.’ ” Naye Sauli akala
pamoja na Samweli siku ile.
25 [b]Baada ya kushuka kutoka mahali pa
juu na kufika mjini, Samweli alizungumza
na Sauli juu ya dari ya nyumba yake.
26 Walipoamka mapema alfajiri, Samweli
akamwita Sauli darini, akamwambia,
“Jiandae, nami nitakuaga uende zako.”
Sauli alipokuwa tayari yeye na Samweli
wakatoka nje pamoja. 27 Hata walipokuwa
wakiteremka kuelekea mwisho wa mji,
Samweli akamwambia Sauli, “Mwambie
mtumishi atangulie mbele yetu.” Naye
mtumishi akafanya hivyo. “Lakini subiri
hapa kwa kitambo kidogo, ili nipate kukupa
ujumbe kutoka kwa Mungu.”

10 [c]Ndipo Samweli akachukua chupa
ndogo ya mafuta na kuyamimina
juu ya kichwa cha Sauli, akambusu,
akisema, “Je, BWANA hakukutia mafuta
uwe kiongozi juu ya watu wake Israeli?
2 [d]Utakapoondoka kwangu leo, utakutana
na watu wawili karibu na kaburi la Raheli,
huko Selsa kwenye mpaka wa Benyamini.
Watakuambia, ‘Punda wale uliotoka kwenda
kuwatafuta, wamekwisha kupatikana. Sasa
baba yako ameacha kufikiri kuhusu punda
na sasa ana hofu kukuhusu wewe. Anauliza,
“Nitafanyaje kuhusu mwanangu?” ’
3 [e]“Kisha utakwenda mbele kutoka hapa
mpaka uufikie mwaloni wa Tabori. Watu
watatu wanaopanda kwa Mungu huko
Betheli watakutana nawe hapo. Mmoja
atakuwa amechukua wana-mbuzi watatu,
mwingine mikate mitatu, na mwingine
kiriba cha divai. 4 [f]Watakusalimu na kukupa
mikate miwili, ambayo utaipokea kutoka
kwao.
5 [g]“Baada ya hayo utakwenda Gibea
ya Mungu, ambapo hapo kuna kambi ya
Wafilisti. Unapokaribia mji utakutana na
kundi la manabii wakiteremka kutoka
mahali pa juu wakiwa na vinubi, matari,
filimbi na zeze vikipigwa mbele yao, nao
watakuwa wakitoa unabii. 6 [h]Roho wa
BWANA atakuja juu yako kwa nguvu, nawe
utatoa unabii pamoja nao; nawe utageuzwa
kuwa mtu wa tofauti. 7 [i]Mara ishara hizi
zitakapotimizwa, fanya lolote mkono
wako upasao kufanya, kwa kuwa Mungu
yu pamoja nawe.
8 [j]“Tangulia kushuka mbele yangu mpaka
Gilgali. Hakika nami nitateremka nikujie ili
kutoa dhabihu za sadaka za kuteketezwa na
dhabihu za amani, lakini lazima ungoje kwa
siku saba hata nitakapokujia na kukuambia
likupasalo kufanya.”

### *Sauli Afanywa Mfalme*

9 [k]Ikawa Sauli alipogeuka kumwacha
Samweli, Mungu aliubadilisha moyo wa
Sauli, na ishara hizi zote zikatimizwa siku
ile. 10 [l]Walipofika Gibea, akakutana na
kundi la manabii. Roho wa Mungu akaja
juu yake kwa nguvu, naye akajiunga
nao katika kutoa unabii kwao. 11 [m]Ikawa
wale wote waliomfahamu hapo mwanzo
walipomwona akitoa unabii pamoja
na manabii, wakaulizana, “Ni nini hiki

[a]**9:24** Law 7:24; Hes 18:18; Eze 24:4; Mdo 10:9
[b]**9:25** Kum 22:8; Yos 2:8; Mt 24:17; Lk 5:19; Mdo 10:9
[c]**10:1** 1Sam 16:1; 9:16; 2Fal 9:1; Kut 29:7; 34:9; 1Sam 9:16; 1Fal 1:39; 2Sam 20:19; Za 78:62-71; Kum 32:9; Yer 10:16
[d]**10:2** Mwa 35:20; 1Sam 9:4-5; Yos 18:28
[e]**10:3** Mwa 35:8; 28:22; Yos 19:22; Amu 4:6, 12; 8:18; Za 89:12
[f]**10:4** 1Sam 16:20; Mit 18:20; Amu 18:15
[g]**10:5** 1Sam 11:4; 15:34; 13:3; Hes 11:29; 1Fal 20:35; 2Fal 2:3; 4:1; 6:1; 9:1; 3:15; Amo 7:14; Law 26:30; Mwa 31:27; Yer 31:4; 1Fal 1:40; Isa 30:29; 1Sam 16:16; 18:10; 19:9; 19:20; Za 92:3; 1Nya 25:1; 1Kor 14:1
[h]**10:6** Hes 11:25; 1Sam 19:23-24; Mt 7:22
[i]**10:7** 2Sam 7:3; 1Fal 8:17; 1Nya 22:7; 28:2; 2Nya 6:7; Mhu 9:10; Amu 9:33; Yos 1:3; Lk 1:28; Ebr 13:5
[j]**10:8** Yos 4:20; 10:43; 1Sam 7:16; 11:14; 13:4
[k]**10:9** Kum 13:2
[l]**10:10** Hes 11:25; 1Sam 11:6; 19:20; Mt 7:21-23
[m]**10:11** Mt 13:54; Yn 7:15; 1Sam 19:24; 2Fal 9:11; Yer 29:26; Hos 9:7

kilichomtokea mwana wa Kishi? Je, Sauli
naye pia yumo miongoni mwa manabii?”
12 [a]Mtu mmoja ambaye aliishi huko
akajibu, “Je, naye baba yao ni nani?” Basi
ikawa mithali, kusema, “Je, Sauli pia yumo
miongoni mwa manabii?” 13 [b]Baada ya Sauli
kumaliza kutoa unabii, alikwenda mahali
pa juu.
14 [c]Basi babaye mdogo akamuuliza Sauli
na mtumishi wake, “Je, mlikuwa wapi?”
Akajibu, “Tulikuwa tukiwatafuta punda.
Lakini tulipoona hawapatikani, tulikwenda
kwa Samweli.”
15 Babaye mdogo Sauli akasema,
“Niambie Samweli amekuambia nini.”
16 [d]Sauli akajibu, “Alituhakikishia
kwamba punda wamepatikana.” Lakini
hakumwambia babaye mdogo kila kitu
Samweli alichomwambia kuhusu ufalme.
17 [e]Samweli akawaita watu wa Israeli
kuja kwa BWANA huko Mispa, 18 [f]naye
akawaambia, “Hili ndilo asemalo BWANA,
Mungu wa Israeli: ‘Niliwatoa Israeli kutoka
Misri, nami niliwaokoa toka nguvu za Misri
na falme zote zilizowaonea.’ 19 [g]Lakini
sasa mmemkataa Mungu wenu, ambaye
anawaokoa toka katika maafa yenu yote
na taabu zenu zote. Nanyi mmesema,
‘Hapana, tuteulie mfalme atutawale.’ Sasa
basi, jihudhurisheni wenyewe mbele za
BWANA kwa kabila zenu na kwa koo zenu.”
20 [h]Samweli alipoyasogeza makabila
yote ya Israeli, kabila la Benyamini
likachaguliwa. 21 [i]Kisha akalisogeza mbele
kabila la Benyamini, ukoo kwa ukoo, nao
ukoo wa Matri ukachaguliwa. Mwishoni
Sauli mwana wa Kishi akachaguliwa. Lakini
walipomtafuta, hakuonekana. 22 [j]Wakazidi
kuuliza kwa BWANA, “Je, huyo mtu
amekwisha kufika hapa?”
Naye BWANA akasema, “Ndiyo,
amejificha katikati ya mizigo.”
23 [k]Wakakimbia na kumleta kutoka
huko, naye aliposimama katikati ya watu,
alikuwa mrefu kuliko watu wengine wote.
24 [l]Samweli akawaambia watu wote,
“Je, mnamwona mtu ambaye BWANA
amemchagua? Hayupo aliye kama yeye
miongoni mwa watu wote.”
Ndipo watu wakapiga kelele, wakasema,
“Mfalme na aishi maisha marefu.”
25 [m]Samweli akawaeleza watu madaraka
ya ufalme. Akayaandika kwenye kitabu na
kuweka mbele za BWANA. Kisha Samweli
akawaruhusu watu, kila mmoja aende
nyumbani kwake.
26 [n]Sauli pia akaenda nyumbani kwake
huko Gibea, akisindikizwa na watu hodari
ambao Mungu alikuwa amegusa mioyo
yao. 27 [o]Lakini baadhi ya watu wakorofi
walisema, “Huyu mtu atawezaje kutuokoa?”
Wakamdharau na wala hawakumletea
zawadi. Lakini Sauli akanyamaza kimya.

*Sauli Aukomboa Mji Wa Yabeshi*

11 [p]Nahashi yule Mwamoni, akakwea
kuuzunguka kwa jeshi mji wa
Yabeshi-Gileadi. Watu wote wa Yabeshi
wakamwambia, “Fanya mkataba na sisi,
na tutakuwa chini yako.”
2 [q]Lakini Nahashi yule Mwamoni akajibu,
“Nitafanya mkataba na ninyi tu kwa sharti
kwamba nitang’oa jicho la kulia la kila

[a]**10:12** Isa 54:13; Yn 3:8
[b]**10:13** 1Sam 19:23
[c]**10:14** 1Sam 14:50; 9:3
[d]**10:16** 1Sam 9:3, 20
[e]**10:17** 1Sam 7:5; Amu 20:1; 1Sam 11:15
[f]**10:18** Kut 1:14; Hes 10:9; Amu 6:8-9; Kum 4:34; Neh 9:9-12
[g]**10:19** Hes 11:20; Kum 33:5; Za 7:10; 18:48; 68:20; 145:19; 1Sam 8:5; Kum 17:14; Yos 7:14
[h]**10:20** Yos 7:14; Mdo 1:24
[i]**10:21** Es 3:7; Mit 16:33
[j]**10:22** Mwa 25:22; Amu 18:5
[k]**10:23** 1Sam 9:2
[l]**10:24** Kum 17:15; 2Sam 21:6; 1Sam 9:2; 1Fal 1:25, 34, 39; 2Fal 11:12
[m]**10:25** 1Sam 8:9; Kum 17:14-20; 1Sam 8:11-18; 2Fal 11:12; 1Sam 11:14
[n]**10:26** Amu 19:14; 20:44
[o]**10:27** Kum 13:13; 1Sam 20:7; 1Fal 10:25; 2Nya 32:23; 17:5; Za 68:29; Mdo 7:35, 51, 52; 2Sam 8:2; 1Fal 4:21; 10:25; Za 72:10; Mt 2:11
[p]**11:1** Mwa 19:38; 1Sam 12:12; 31:11; 2Sam 10:2; 17:27; 2:4-5; 21:12; Kut 23:32; Yer 37:1; Eze 17:13; 1Nya 19:1; Amu 21:8
[q]**11:2** Mwa 34:15; Hes 16:14; 1Sam 17:26; 2Sam 17:26

mmoja wenu, na hivyo kuleta aibu juu ya
Israeli yote."
3 [a]Viongozi wa Yabeshi wakamwambia,
"Tupe siku saba ili tuweze kutuma wajumbe
katika Israeli yote, kama hakuna hata
mmoja anayekuja kutuokoa, tutajisalimisha
kwako."
4 [b]Wajumbe walipofika Gibea ya Sauli na
kutoa taarifa juu ya masharti haya kwa watu,
wote walilia kwa sauti kubwa. 5 Wakati
huo huo Sauli alikuwa anarudi kutoka
mashambani, akiwa nyuma ya maksai
wake, naye akauliza, "Watu wana nini?
Mbona wanalia?" Ndipo wakamweleza jinsi
watu wa Yabeshi walivyokuwa wamesema.
6 [c]Sauli aliposikia maneno yao, Roho
wa Mungu akaja juu yake kwa nguvu,
naye akawaka hasira. 7 [d]Akachukua jozi
ya maksai na kuwakata vipande vipande,
naye kuvituma hivyo vipande kupitia
wajumbe katika Israeli yote, wakitangaza,
"Hivi ndivyo itakavyofanyika kwa maksai
wa kila mmoja ambaye hatamfuata Sauli
na Samweli." Kisha hofu ya BWANA
ikawaangukia watu, nao wakatoka kama
mtu mmoja. 8 [e]Sauli alipowakusanya huko
Bezeki, watu wa Israeli walikuwa 300,000
na watu wa Yuda 30,000.
9 Wakawaambia wale wajumbe
waliokuwa wamekuja, "Waambieni watu
wa Yabeshi-Gileadi, 'Kesho kabla jua
halijawa kali, mtaokolewa.'" Wajumbe
walipokwenda na kutoa taarifa hii kwa watu
wa Yabeshi, wakafurahi. 10 Wakawaambia
Waamoni, "Kesho tutajisalimisha kwenu,
nanyi mtaweza kututendea chochote
mnachoona chema kwenu."
11 [f]Kesho yake Sauli alitenganisha watu
wake katika vikosi vitatu; wakati wa zamu
ya mwisho ya usiku wakaingia katika kambi
ya Waamoni na kuwachinja mpaka mchana.
Wale walionusurika wakasambaa, kiasi
kwamba hawakusalia watu wawili pamoja.

*Sauli Athibitishwa Kuwa Mfalme*

12 [g]Kisha watu wakamwambia Samweli,
"Ni nani yule aliyeuliza, 'Je, Sauli atatawala
juu yetu?' Tuletee hawa watu, nasi
tutawaua."
13 [h]Lakini Sauli akasema, "Hakuna hata
mmoja atakayeuawa leo, kwa kuwa siku
hii BWANA ameokoa Israeli."
14 [i]Ndipo Samweli akawaambia watu,
"Njooni, twendeni Gilgali na huko
tuthibitishe ufalme." 15 [j]Kwa hiyo watu
wote wakaenda Gilgali na kumthibitisha
Sauli kuwa mfalme mbele za BWANA. Huko
wakatoa dhabihu za sadaka za amani mbele
za BWANA, naye Sauli na Waisraeli wote
wakafanya karamu kubwa.

*Hotuba Ya Samweli Ya Kuaga*

12 [k]Samweli akawaambia Israeli wote,
"Nimesikiliza kila kitu mlichoniambia
nami nimewawekea mfalme juu yenu.
2 [l]Sasa mnaye mfalme kama kiongozi
wenu. Lakini kwa habari yangu mimi ni
mzee na nina mvi, nao wanangu wapo
hapa pamoja nanyi. Nimekuwa kiongozi
wenu tangu ujana wangu mpaka siku hii ya
leo. 3 [m]Mimi ninasimama hapa. Shuhudieni
juu yangu mbele za BWANA na mpakwa
mafuta wake. Nimechukua maksai wa
nani? Nimechukua punda wa nani? Ni nani
nimepata kumdanganya? Ni nani nimepata
kumwonea? Ni kutoka kwenye mkono
wa nani nimepokea rushwa ili kunifanya
nifumbe macho yangu? Kama nimefanya
chochote katika hivi, mimi nitawarudishia."
4 Wakajibu, "Hujatudanganya wala

[a]**11:3** 1Sam 8:4; Amu 2:16
[b]**11:4** 1Sam 10:5; 15:34; Mwa 27:38; Hes 25:6; Amu 2:4; 21:2; 2Sam 21:6; Rum 12:15
[c]**11:6** Amu 3:10; 6:34; 13:25; 1Sam 10:10; 16:13
[d]**11:7** 1Sam 6:14; Amu 19:29; 21:5; 20:1; Mwa 35:5; 1Nya 14:14; 17:10; Mit 14:26
[e]**11:8** Amu 20:2; 1:4; 2Sam 24:9
[f]**11:11** Amu 7:16; Mwa 19:38
[g]**11:12** Kum 13:13; Lk 19:27
[h]**11:13** 2Sam 19:22; 1Sam 19:5; 1Nya 11:14; Kut 14:13; Za 44:4-8; Ebr 2:3
[i]**11:14** Yos 10:43; 1Sam 10:8; 10:25
[j]**11:15** Yos 5:9; 2Sam 19:15; 1Sam 12:1
[k]**12:1** 1Sam 8:7; 11:15; 10:25
[l]**12:2** 1Sam 8:5; 8:3; Hes 27:17
[m]**12:3** 1Sam 9:16; 24:6; 26:9-11; 2Sam 1; 14; 19:21; Za 105:15; Hes 16:15; Kut 18:21; 20:17; 1Sam 8; 3; Mdo 20:33; Law 25:14; Kum 16:19

kutuonea. Hujapokea chochote kutoka
kwenye mkono wa mtu awaye yote.”
5 [a]Samweli akawaambia, “Bwana ni
shahidi juu yenu, pia mpakwa mafuta
wake ni shahidi siku hii ya leo, kwamba
hamkukuta chochote mkononi mwangu.”
Wakasema, “Yeye ni shahidi.”
6 [b]Kisha Samweli akawaambia watu,
“Bwana ndiye alimchagua Mose na Aroni,
na kuwaleta baba zenu akiwapandisha
kutoka Misri. 7 [c]Sasa basi, simameni hapa,
kwa sababu nitakabiliana nanyi kwa
ushahidi mbele za Bwana wa matendo yote
ya haki yaliyofanywa na Bwana kwenu na
kwa baba zenu.
8 [d]“Baada ya Yakobo kuingia Misri,
walimlilia Bwana kwa ajili ya msaada,
naye Bwana akawatuma Mose na Aroni,
ambao waliwatoa baba zenu kutoka Misri
na kuwakalisha mahali hapa.
9 [e]“Lakini wakamsahau Bwana Mungu
wao, hivyo Mungu akawauza katika
mkono wa Sisera, jemadari wa jeshi la
Hazori na katika mikono ya Wafilisti na
mfalme wa Moabu, ambaye alipigana dhidi
yao. 10 [f]Wakamlilia Bwana na kusema,
‘Tumetenda dhambi; tumemwacha Bwana
na kutumikia Mabaali na Maashtorethi.
Lakini sasa tuokoe kutoka mikono ya adui
zetu, nasi tutakutumikia.’ 11 [g]Ndipo Bwana
akawatuma Yerub-Baali,[h] Baraka, Yefta na
Samweli, naye akawaokoa kutoka mikononi
mwa adui zenu kila upande, ili ninyi mpate
kukaa salama.
12 [i]“Lakini mlipomwona yule Nahashi
mfalme wa Waamoni anakuja dhidi yenu,
mliniambia, ‘Hapana, tunataka mfalme
atutawale,’ hata ingawa Bwana Mungu
wenu alikuwa mfalme wenu. 13 [j]Sasa huyu
hapa ndiye mfalme mliyemchagua, yule
mliyeomba; tazameni, Bwana amemweka
mfalme juu yenu. 14 [k]Kama mkimcha Bwana
na kumtumikia na kumtii nanyi msipoasi
dhidi ya amri zake, ninyi pamoja na
mfalme anayetawala juu yenu mkimfuata
Bwana, Mungu wenu, mambo yatakuwa
mema kwenu! 15 [l]Lakini kama hamkumtii
Bwana, nanyi kama mkiasi dhidi ya amri
zake, mkono wake utakuwa dhidi yenu,
kama ulivyokuwa dhidi ya baba zenu.
16 [m]“Sasa basi, simameni kimya mkaone
jambo hili kubwa ambalo Bwana
anakwenda kulifanya mbele ya macho
yenu! 17 [n]Je, sasa si mavuno ya ngano?
Nitamwomba Bwana ili alete ngurumo
na mvua. Nanyi mtatambua jambo hili
lilivyo baya mlilolifanya mbele za macho
ya Bwana mlipoomba mfalme.”
18 [o]Kisha Samweli akamwomba Bwana,
na siku ile ile Bwana akatuma ngurumo
na mvua. Hivyo watu wote wakamwogopa
sana Bwana na Samweli.
19 [p]Watu wote wakamwambia Samweli,
“Mwombe Bwana Mungu wako kwa ajili
ya watumishi wako, ili tusije tukafa, kwa
kuwa tumeongeza uovu juu ya dhambi zetu
nyingine kwa kuomba mfalme.”
20 [q]Samweli akajibu, “Msiogope,
mmefanya uovu huu wote; hata hivyo
msimwache Bwana, bali mtumikieni

[a]**12:5** Mwa 31:50; Mdo 23:9; 24:20; Kut 22:4; Yn 18:38; 2Kor 1:12; Za 17:3
[b]**12:6** Kut 6:26; 3:10; Mik 6:4; Neh 9:9-14; 2Kor 1:12; Za 17:3
[c]**12:7** Yos 24:1; Isa 1:18; 3:14; Yer 2:9; 25:31; Eze 17:20; 20:35; Mik 6:1-5; Amu 5; 11
[d]**12:8** Mwa 46:6; Kut 2:23; 3:10; 4:16
[e]**12:9** Kum 32:18; 32:30; Amu 3:7; 4:2; 10:7; 3:12; 13:1; Yos 11:1
[f]**12:10** Amu 3:9; 2:13; 10:10, 15; 1Sam 8:8; 7:3
[g]**12:11** Amu 6:32; 4:6; 11:1; 1Sam 7:15
[h]11 Yerub-Baali pia aliitwa Gideoni.
[i]**12:12** 1Sam 11:1; 8:5; 25:30; 1Nya 5:2; 2Sam 5:2; Amu 8:3-23
[j]**12:13** 1Sam 8:5; 9:20; 10:24; Hos 13:11
[k]**12:14** Yos 24:14; Yer 4:17; Mao 1:18; Kum 6:13; 10:12; 13:4; Yos 24:14; Za 81:13; Mhu 8:12; Isa 3:10
[l]**12:15** Law 26:16; Yos 24:20; Isa 1:20; Yer 4:17; 26:4
[m]**12:16** Kut 14:13-14
[n]**12:17** Mwa 30:14; 7:12; 1Sam 6:13; 2:10; 1Fal 18:42; Yak 5:18; Kut 9:23; 9:18; Ay 37:13; Mit 26:1; 1Sam 8:6-7; 7:9-10
[o]**12:18** Za 99:8; Mwa 3:10; Kut 14:31
[p]**12:19** Kut 8:8; 1Sam 7:8; Yer 37:3; Yak 5:18; 1Yn 5:16
[q]**12:20** Kum 32:30

BWANA kwa moyo wenu wote. 21 [a]Msigeukie
sanamu zisizofaa. Haziwezi kuwatendea
jema, wala haziwezi kuwaokoa kwa
sababu hazina maana. 22 [b]Kwa ajili ya
jina lake kuu BWANA hatawakataa watu
wake, kwa sababu ilimpendeza BWANA
kuwafanya kuwa wake mwenyewe. 23 [c]Kwa
habari yangu, iwe mbali nami kutenda
dhambi dhidi ya BWANA kwa kushindwa
kuwaombea. Mimi nitawafundisha njia iliyo
njema na ya kunyooka. 24 [d]Lakini hakikisheni
mnamcha BWANA na kumtumikia kwa
uaminifu kwa moyo wenu wote; tafakarini
mambo makubwa aliyoyatenda kwa ajili
yenu. 25 [e]Hata hivyo mkiendelea kufanya
uovu, ninyi na mfalme wenu mtafutiliwa
mbali!”

*Samweli Amkemea Sauli*

13 Sauli alikuwa na miaka thelathini,
alipokuwa mfalme, akatawala Israeli
miaka arobaini na miwili.

2 [f]Sauli alichagua watu 3,000 kutoka
Israeli; miongoni mwa hao watu 2,000
walikuwa pamoja naye huko Mikmashi
na katika nchi ya vilima ya Betheli, nao
watu 1,000 walikuwa pamoja na Yonathani
huko Gibea ya Benyamini. Watu waliosalia
aliwarudisha nyumbani mwao.

3 [g]Yonathani akashambulia ngome ya
Wafilisti huko Geba, nao Wafilisti wakapata
habari hizo. Kisha Sauli akaamuru
tarumbeta ipigwe nchi yote na kusema,
“Waebrania na wasikie!” 4 [h]Hivyo Israeli
wote wakasikia habari kwamba: “Sauli
ameshambulia ngome ya Wafilisti, nao
sasa Israeli wamekuwa harufu mbaya kwa
Wafilisti.” Basi watu waliitwa kuungana na
Sauli huko Gilgali.

5 [i]Wafilisti wakakusanyika ili kupigana
na Israeli, wakiwa na magari ya vita 3,000,
waendesha magari ya vita 6,000 na askari
wa miguu wengi kama mchanga wa ufuoni
mwa bahari. Walipanda na kupiga kambi
huko Mikmashi, mashariki ya Beth-Aveni.
6 [j]Watu wa Israeli walipoona kuwa hali yao
ni ya hatari na kuwa jeshi lao limesongwa
sana, wakajificha katika mapango na katika
vichaka, katikati ya miamba, kwenye
mashimo na kwenye mahandaki. 7 [k]Hata
baadhi ya Waebrania wakavuka Yordani
mpaka nchi ya Gadi na Gileadi.

Sauli akabaki huko Gilgali, navyo vikosi
vyote vilivyokuwa pamoja naye vilikuwa
vikitetemeka kwa hofu. 8 [l]Akangoja kwa siku
saba, muda uliowekwa na Samweli; lakini
Samweli hakuja Gilgali, nao watu wa Sauli
wakaanza kutawanyika. 9 [m]Basi akasema,
“Nileteeni hapa sadaka ya kuteketezwa na
sadaka za amani.” Naye Sauli akatoa sadaka
ya kuteketezwa. 10 [n]Mara alipomaliza kutoa
hiyo sadaka, Samweli akatokea, naye Sauli
akaondoka kwenda kumlaki.

11 Samweli akamuuliza, “Umefanya
nini?”

Sauli akajibu, “Nilipoona kwamba
watu wanatawanyika, na kwamba hukuja
wakati uliopangwa na kwamba Wafilisti
walikuwa wakikusanyika huko Mikmashi,
12 [o]nikawaza, ‘Sasa Wafilisti watateremka
dhidi yangu huko Gilgali nami sijaomba
kibali kwa BWANA.’ Hivyo nikalazimika
kutoa sadaka ya kuteketezwa.”

[a]**12:21** Isa 40:20; 41:24-29; 44:9; Yer 2:5, 11; 14:22; 16:19; Yn 2:8; Hab 2:8; Mdo 14:15; Kum 11:16
[b]**12:22** Za 25:11; 106:8; Isa 48:9-11; Yer 14:7; Dan 9:19; Yos 7:9; 2Sam 7:23; Yn 17:12; Law 26:11; Kum 31:6; 7:7; 1Pet 2:6; 1Fal 6:13
[c]**12:23** Hes 11:2; 1Sam 1:20; 7:2; Rum 1:10; 1Fal 8:36; Za 25:4; 34:11; 86:11; 94:12; Mit 4:11; Kol 1:9
[d]**12:24** Kum 6:2; Mhu 12:13; Kum 6:5; Yos 24:14; Ay 34:27; Isa 5:12; 22:11; 26:10; Kum 10:21
[e]**12:25** 1Sam 31:1-5; Kum 28:36; Yos 24:20; 1Fal 14:10
[f]**13:2** Neh 11:31; Isa 10:28; Amu 19:14; 1Sam 10:26
[g]**13:3** 1Sam 10:5; Yos 18:24; Law 25:6; Amu 3:27
[h]**13:4** Mwa 34:30
[i]**13:5** 1Sam 17:1; Yos 11:4; Ufu 20:8; Yos 7:2
[j]**13:6** 1Sam 14:11, 22; Amu 6:2; Eze 33:27
[k]**13:7** Hes 32:33; Mwa 35:5; Kut 19:16
[l]**13:8** 1Sam 10:8
[m]**13:9** Kum 12:5-14; 2Sam 24:25; 1Fal 3:4; 2Nya 26:16; Mit 15:8; 21:3, 27; Ebr 5:4
[n]**13:10** 1Sam 15:13; 25:14; Rut 2:4
[o]**13:12** Yos 10:43; Kum 4:29; Za 119:58; Yer 26:19

13 [a]Samweli akasema, “Umetenda kwa
upumbavu. Hukuyashika maagizo ya
BWANA Mungu wako aliyokupa. Kama
ungelitii, angeudumisha ufalme wako
juu ya Israeli kwa wakati wote. 14 [b]Lakini
sasa ufalme wako hautadumu; BWANA
amemtafuta mtu aupendezaye moyo wake,
na amemchagua awe kiongozi wa watu
wake, kwa sababu hukuyatii maagizo ya
BWANA.”
15 [c]Kisha Samweli akaondoka Gilgali,
akapanda Gibea ya Benyamini, naye Sauli
akawahesabu watu aliokuwa nao. Jumla
yao walikuwa watu 600.

*Israeli Bila Silaha*

16 [d]Sauli, mwanawe Yonathani na watu
waliokuwa pamoja nao walikuwa wakiishi
huko Gibea ya Benyamini, wakati Wafilisti
wakiwa wamepiga kambi huko Mikmashi.
17 [e]Makundi ya wavamiaji walikuja kutoka
kambi ya Wafilisti katika vikosi vitatu.
Kikosi kimoja kilielekea Ofra karibu na
Shuali, 18 [f]kikosi kingine kilielekea Beth-
Horoni, nacho kikosi cha tatu kilielekea
kwenye nchi ya mpakani ielekeayo Bonde
la Seboimu linalotazamana na jangwa.
19 [g]Hapakuwa na mhunzi ambaye
angeweza kupatikana katika nchi
yote ya Israeli, kwa sababu Wafilisti
walikuwa wamesema, “Waebrania wasije
wakatengeneza panga au mikuki!” 20 Hivyo
Waisraeli wote huteremka kwa Wafilisti
ili kunoa majembe ya plau, majembe ya
mkono, mashoka na miundu. 21 Bei ilikuwa
fedha theluthi mbili za shekeli[h] kunoa
majembe ya plau na majembe ya mkono,
na theluthi moja ya shekeli[i] kwa nyuma,
mashoka na michokoo.
22 [j]Kwa hiyo siku ya vita hakuna askari
yeyote aliyekuwa kambini na Sauli na
Yonathani ambaye alikuwa na upanga
wala mkuki mkononi mwake; Sauli tu
na mwanawe Yonathani ndio waliokuwa
navyo.

*Yonathani Awashambulia Wafilisti*

23 [k]Basi kikosi cha Wafilisti kilikuwa
kimetoka kuelekea njia iendayo Mikmashi.
14 Siku moja Yonathani mwana wa Sauli
akamwambia kijana mbeba silaha wake,
akasema, “Njoo, tuwavukie Wafilisti
kwenye doria upande ule mwingine.” Lakini
hakumwambia baba yake.
2 [l]Sauli alikuwa akikaa kwenye viunga
vya Gibea chini ya mkomamanga huko
Migroni. Alikuwa pamoja na watu kama
600, 3 [m]miongoni mwao alikuwepo Ahiya,
ambaye alikuwa amevaa kisibau. Alikuwa
mwana wa Ikabodi, nduguye Ahitubu
mwana wa Finehasi, mwana wa Eli, kuhani
wa BWANA huko Shilo. Hakuna yeyote
aliyekuwa na habari kwamba Yonathani
alikuwa ameondoka.
4 [n]Kila upande wa njia ambayo Yonathani
alikusudia kupita ili kuvuka kufikia doria
ya Wafilisti kulikuwepo na jabali; moja
lilikuwa linaitwa Bosesi, na jingine Sene.
5 [o]Jabali moja lilisimama kaskazini kuelekea
Mikmashi na jingine upande wa kusini
kuelekea Geba.

[a]**13:13** 2Nya 16:9; Yos 22:16; 1Sam 15:23, 24; 2Sam 7:15; 1Nya 10:13; Za 72:5; 1Fal 18:18; Ay 34:18; Mit 19:3; Mt 14:3, 4; Law 17:1; Hes 18:7
[b]**13:14** 1Sam 15:28; 18:8; 24:20; 1Nya 10:14; Mdo 7:46; 13:12; 2Sam 6:21; 1Sam 25:10; 2Sam 5:2; Za 18:43; Isa 16:5; 55:4; Yer 30:9; Eze 34:23-24; 37:24; Dan 9:25; Hos 3:5; Mik 5:2; 1Sam 15:26; 16; 1; 2Sam 12:6; 1Fal 13:21
[c]**13:15** 1Sam 14:2
[d]**13:16** Yos 18:24
[e]**13:17** 1Sam 14:15; Yos 18:23
[f]**13:18** Yos 10:10; Neh 11:34; Yos 18:13-14; 1Nya 6:68; 2Nya 8:5
[g]**13:19** Mwa 4:22; Hes 25:7; Yer 24:1; 2Fal 24:14
[h]21 Theluthi mbili za shekeli za fedha ni sawa na gramu 8.
[i]21 Theluthi moja ya shekeli ya fedha ni sawa na gramu 4.
[j]**13:22** 1Nya 9:39; Hes 25:7; 1Sam 14:6; 17:47; Zek 4:6; Amu 5:8
[k]**13:23** 1Sam 14:4
[l]**14:2** Amu 4:5; 1Sam 13:15; Kut 28:33; Isa 10:28
[m]**14:3** Mwa 35:18; 1Sam 22:11; 1:3; Za 78:60; 1Sam 4:21; 2:28; 4:21; Kut 28:30; 1Sam 2:28; 22:18
[n]**14:4** 1Sam 13:23
[o]**14:5** Yos 18:24

6 [a]Yonathani akamwambia kijana wake
mbeba silaha, “Njoo, tuvukie doria ya wale
jamaa wasiotahiriwa. Huenda BWANA
atatenda kwa ajili yetu. Hakuna chochote
kitakachoweza kumzuia BWANA kuokoa,
kwamba ni kwa wingi au kwa uchache.”
7 Mbeba silaha wake akamwambia,
“Fanya yale yote uliyo nayo katika moyo
wako. Songa mbele; moyo wangu na roho
yangu viko pamoja nawe.”
8 Yonathani akasema, “Basi njoo;
tutavuka kuwaelekea hao watu na kuacha
watuone. 9 Kama wakituambia, ‘Subirini
hapo mpaka tuje kwenu,’ tutakaa pale
tulipo na hatutakwea kwao. 10 [b]Lakini
kama watasema, ‘Pandeni mje kwetu,’
tutakwea, kwa sababu hiyo itakuwa ishara
yetu kwamba BWANA amewatia mikononi
mwetu.”
11 [c]Basi wote wawili wakajionyesha kwa
doria ya Wafilisti. Wafilisti wakasema,
“Tazama! Waebrania wanatambaa toka
mashimoni walimokuwa wamejificha.”
12 [d]Watu wa kwenye doria wakawapigia
kelele Yonathani na mbeba silaha wake,
wakisema, “Njooni, pandeni kwetu nasi
tutawakomesha.”
Basi Yonathani akamwambia mbeba
silaha wake, “Panda nyuma yangu; BWANA
amewatia mikononi mwa Israeli.”
13 Yonathani akapanda juu, akitumia
mikono yake na miguu, pamoja na mbeba
silaha wake papo hapo nyuma yake.
Wafilisti wakaanguka mbele ya Yonathani,
naye mbeba silaha wake akamfuata akiwaua
nyuma yake. 14 Katika hilo shambulio la
kwanza, Yonathani na mbeba silaha wake
waliua kama watu ishirini kwenye eneo
kama la nusu eka.

*Israeli Wawafukuza Wafilisti*

15 [e]Kisha fadhaa ikawapata jeshi lote,
wale waliokuwa kambini na shambani,
wale waliokuwa katika doria na makundi
ya washambuliaji, nayo nchi ilitetemeka.
Ilikuwa ni hofu ya ghafula iliyotumwa na
Mungu.
16 [f]Wapelelezi wa Sauli huko Gibea ya
Benyamini wakaona jeshi likitokomea
pande zote. 17 Ndipo Sauli akawaambia watu
wale waliokuwa pamoja naye, “Kagueni
jeshi mkaone ni nani ameondoka katikati
yetu.” Walipokagua, akawa ni Yonathani
na mbeba silaha wake ambao hawakuwepo.
18 [g]Sauli akamwambia Ahiya, “Leta
Sanduku la Mungu.” (Wakati huo lilikuwa
kwa Waisraeli.) 19 [h]Wakati Sauli alipokuwa
akisema na kuhani, makelele katika kambi
ya Wafilisti yakaongezeka zaidi na zaidi.
Hivyo Sauli akamwambia kuhani, “Rudisha
mkono wako.”
20 [i]Kisha Sauli na watu wake wote
wakakusanyika na kwenda vitani.
Wakawakuta Wafilisti wakiwa
wamechanganyikiwa kabisa, wakitiana
panga kila mmoja na wenzake. 21 [j]Wale
Waebrania ambao walishakuwa pamoja
na Wafilisti, na waliokuwa wamepanda
pamoja nao katika kambi zao, wakaenda
upande wa Waisraeli waliokuwa pamoja
na Sauli na Yonathani. 22 [k]Waisraeli wote
waliokuwa wamejificha katika nchi ya
milima ya Efraimu waliposikia kuwa
Wafilisti wamekimbia, wakajiunga vitani
na kuwafuata kwa bidii. 23 [l]Hivyo BWANA
akawaokoa Waisraeli siku ile, navyo vita
vilienea hadi kupita Beth-Aveni.

---

[a]**14:6** Amu 14:3; 1Sam 17:26; 31:4; Yer 9:26; Eze 28:10; 1Sam 13:22; 1Fal 19:12; Mt 19:26; Ebr 11:34; Amu 7:4; Za 33:16; 1Sam 17:46-47
[b]**14:10** Mwa 24:1, 14; Yos 2:24; Amu 6:36-37; 1Sam 10:7; 2Sam 5:24; Isa 7:11-14
[c]**14:11** Mwa 14:13; 1Sam 13:6
[d]**14:12** Amu 8:16; 1Sam 17:46; 2Sam 5:24; 1Sam 17:43-44
[e]**14:15** Mwa 35:5; Kut 14:24; 19:16; 2Fal 7:5-7; 1Sam 13:17; Amu 7:21; Ay 18:11; Za 48:5-6
[f]**14:16** 2Sam 18:24; 2Fal 9:17; Isa 52:8; Eze 33:2
[g]**14:18** 1Sam 30:7; Amu 18:5
[h]**14:19** Hes 27:21; Yos 9:14; Za 106:13
[i]**14:20** Amu 7:22; Eze 38:21; Zek 14:13; 2Nya 20:23
[j]**14:21** 1Sam 29:4
[k]**14:22** 1Sam 13:6; Isa 9:19-21
[l]**14:23** Kut 14:30; Yos 7; 2; 1Sam 13:5; Za 44:6-7; Isa 63:9; Za 17:7

*Yonathani Ala Asali*

24 [a]Basi watu wa Israeli walikuwa katika
dhiki siku ile, kwa sababu Sauli alikuwa
amewafunga watu kwa kiapo, akisema,
“Alaaniwe mtu yeyote ambaye atakula
chakula kabla ya jioni, kabla sijalipiza
kisasi juu ya adui zangu!” Kwa hiyo hakuna
mtu yeyote katika jeshi aliyeonja chakula.
25 [b]Jeshi lote liliingia mwituni, na huko
kulikuwepo na asali ardhini. 26 Walipoingia
mwituni, wakaona asali ikitiririka, hata
hivyo hakuna mtu yeyote aliyetia mkono
wake kinywani, kwa sababu waliogopa
kiapo. 27 [c]Lakini Yonathani alikuwa hajasikia
kuwa baba yake alikuwa amewafunga watu
kwa kiapo, hivyo akainyoosha ncha ya fimbo
iliyokuwa mkononi mwake na kuichovya
katika sega la asali. Akainua mkono wake
na kuutia kinywani mwake, nayo macho
yake yakawa maangavu. 28 Kisha mmoja
wa askari wake akamwambia, “Baba yako
alilifunga jeshi kwa kiapo kikali, akisema,
‘Alaaniwe mtu yeyote alaye chakula leo!’
Ndiyo sababu watu wanalegea.”
29 [d]Yonathani akasema, “Baba yangu
ameitaabisha nchi. Ona jinsi nilivyopata
nguvu mpya nilipoonja asali hii kidogo.
30 Ingekuwa bora zaidi mara ngapi kama
watu wangalikula leo baadhi ya nyara
walizoteka kutoka kwa adui zao. Je, mauaji
ya Wafilisti yasingekuwa makubwa zaidi?”
31 [e]Siku ile baada ya Waisraeli kuwaua
Wafilisti kutoka Mikmashi mpaka Aiyaloni,
walikuwa wamechoka. 32 [f]Watu wakarukia
zile nyara, wakichukua kondoo, ng’ombe
na ndama, wakawachinja hapo juu ya nchi
na kuwala, pamoja na damu. 33 [g]Kisha mtu
mmoja akamwambia Sauli, “Tazama, watu
wanatenda dhambi dhidi ya Bwana kwa
kula nyama yenye damu.”
Akasema, “Mmevunja uaminifu.
Livingirisheni jiwe kubwa hapa mara
moja.” 34 [h]Kisha Sauli akasema, “Nendeni
miongoni mwa watu, mwaambie, ‘Kila
mmoja wenu aniletee ng’ombe wake na
kondoo, mwachinjie hapa na mle. Msitende
dhambi dhidi ya Bwana kwa kula nyama
ikiwa na damu ndani yake.’ ”
Hivyo kila mmoja akaleta ng’ombe wake
jioni ile na kumchinja hapo. 35 [i]Ndipo Sauli
akamjengea Bwana madhabahu, na ndiyo
ilivyokuwa mara yake ya kwanza kujenga
madhabahu.
36 [j]Sauli akasema, “Tuteremke tufuatie
Wafilisti usiku na kuwateka nyara mpaka
mapambazuko, nasi tusiache hata mmoja
wao hai.”
Wakajibu, “Fanya lolote lile uonalo jema
zaidi kwako.”
Lakini kuhani akasema, “Tuulize kwa
Mungu mahali hapa.”
37 [k]Basi Sauli akamuuliza Mungu, akisema,
“Je, niteremke kuwafuatia Wafilisti? Je,
utawatia mikononi mwa Israeli?” Lakini
Mungu hakumjibu siku ile.
38 [l]Kwa hiyo Sauli akasema, “Njooni
hapa, ninyi nyote ambao ni viongozi wa
jeshi, na tutafute ni dhambi gani imefanywa
leo. 39 [m]Kwa hakika kama Bwana aiokoaye
Israeli aishivyo, hata kama itakuwa juu ya
mwana wangu Yonathani, ni lazima afe.”
Lakini hakuna mtu yeyote aliyesema neno.
40 Kisha Sauli akawaambia Waisraeli
wote, “Ninyi simameni huko; mimi na
mwanangu Yonathani tutasimama hapa.”
Watu wakajibu, “Fanya lile unaloona
jema zaidi kwako.”
41 [n]Kisha Sauli akamwomba Bwana,
Mungu wa Israeli, akisema, “Nipe jibu lililo
sawa.” Yonathani na Sauli wakatolewa kwa

---

[a]**14:24** Yos 6:26; Law 27:29; Hes 21:2; Kum 27:15-26; Amu 11:30; 21:1-5; Mit 11:9
[b]**14:25** Kum 9:28; Mt 3:5; Kut 3:8; Hes 13:27
[c]**14:27** Za 19:10; Mit 16:24; 24:13
[d]**14:29** Yos 7:25; 1Fal 18:18
[e]**14:31** Yos 10:12
[f]**14:32** 1Sam 15:19; Es 9:10; Mwa 9:4; Law 3:17; Kum 12:16
[g]**14:33** Mwa 9:4
[h]**14:34** Law 19:26
[i]**14:35** 1Sam 7:17; Amu 21:4; 2Sam 24:25
[j]**14:36** Mwa 25:22; Amu 18:5; Mal 2:7; Yak 4:8
[k]**14:37** 1Sam 28:6, 15; 2Sam 22:42; Za 18:41
[l]**14:38** Yos 7:11; 1Sam 10:19
[m]**14:39** Hes 14:21; 2Sam 12:5; Ay 19:25; Za 18:46; 42:2; Yos 7:15
[n]**14:41** Mdo 1:24; Mit 16:33; Yos 7:16; 1Sam 10:20-21

kura, nao watu wakakawa salama. 42 [a]Sauli
akasema, “Pigeni kura kati yangu na
mwanangu Yonathani.” Kura ikamwangukia
Yonathani.
43 [b]Basi Sauli akamwambia Yonathani,
“Niambie ni nini ulichokifanya.”
Hivyo Yonathani akamwambia, “Nilionja
tu asali kidogo kwa ncha ya fimbo yangu.
Je, sasa ni lazima nife?”
44 [c]Sauli akasema, “Mungu na
anishughulikie kwa ukali zaidi kama wewe
Yonathani hutakufa.”
45 [d]Lakini watu wakamwambia Sauli, “Je,
Yonathani atakufa, yeye ambaye ameleta
wokovu huu mkubwa Israeli? Hasha!
Hakika kama Bwana aishivyo, hakuna hata
unywele wa kichwa chake utakaoanguka
juu ya ardhi, kwa kuwa alifanya jambo
hili leo kwa msaada wa Mungu.” Basi watu
wakamwokoa Yonathani, wala hakuuawa.
46 Kisha Sauli akaacha kuwafuata
Wafilisti, nao wakajiondoa na kurudi katika
nchi yao.
47 [e]Baada ya Sauli kujitwalia utawala
katika Israeli, alipigana dhidi ya adui zake
kila upande: Moabu, Waamoni, Edomu,
wafalme wa Soba, na Wafilisti. Popote
alipogeukia, aliwashinda. 48 [f]Akapigana
kishujaa na kuwashinda Waamaleki,
akiikomboa Israeli kutoka mikono ya wale
waliokuwa wamewateka nyara.

*Jamaa Ya Sauli*

49 [g]Wana wa Sauli walikuwa Yonathani,
Ishvi na Malki-Shua. Jina la binti yake
mkubwa lilikuwa Merabu, naye mdogo
aliitwa Mikali. 50 [h]Jina la mkewe Sauli
aliitwa Ahinoamu binti wa Ahimaasi. Jina
la jemadari wa jeshi la Sauli aliitwa Abneri
mwana wa Neri, naye Neri alikuwa babaye
mdogo Sauli. 51 [i]Babaye Sauli yaani, Kishi
na Neri baba yake Abneri walikuwa wana
wa Abieli.
52 [j]Siku zote za utawala wa Sauli zilikuwa
za vita vikali dhidi ya Wafilisti, na wakati
wowote Sauli alimwona mtu mwenye nguvu
au shujaa, alimchukua kwa utumishi wake.

*Bwana Anamkataa Sauli Asiwe Mfalme*

15 [k]Samweli akamwambia Sauli, “Mimi
ndiye ambaye Bwana alinituma
nikutie mafuta uwe mfalme juu ya
watu wake Israeli, basi sasa sikiliza
ujumbe kutoka kwa Bwana. 2 [l]Hili ndilo
Bwana Mwenye Nguvu Zote asemalo:
‘Nitawaadhibu Waamaleki kwa kile
walichowatendea Israeli walipowavizia
wakati walipanda kutoka Misri. 3 [m]Basi
sasa nenda ukawashambulie Waamaleki
na kuwaangamiza kabisa pamoja na kila
kitu kilicho mali yao. Usiwahurumie;
waue wanaume na wanawake, watoto na
wanyonyao, ng’ombe na kondoo, ngamia
na punda.’ ”
4 [n]Ndipo Sauli akawaita watu na
kuwapanga huko Telaimu, askari wa
miguu 200,000 pamoja na watu 10,000
kutoka Yuda. 5 Sauli akaenda katika mji
wa Amaleki na kuwavizia bondeni. 6 [o]Kisha
akawaambia Wakeni, “Ondokeni, waacheni
Waamaleki ili nisije nikawaangamiza ninyi
pamoja nao, kwa kuwa ninyi mliwatendea
mema Waisraeli wote wakati walipanda
kutoka Misri.” Basi Wakeni wakaondoka,
wakawaacha Waamaleki.

[a]**14:42** Yon 1:7
[b]**14:43** Yos 7:19
[c]**14:44** Rut 1:17
[d]**14:45** 1Fal 1:52; Mt 10:30; 2Sam 14:11; Lk 21:18; Isa 13:3; 2Kor 6:1
[e]**14:47** Mwa 19:37-38; 2Sam 12:31; 8:3; 10:6; 23:36
[f]**14:48** Mwa 36:12; Hes 13:29; Amu 3:13; 1Sam 15:2, 7; 27:8; 28:18; 30:13; 2Sam 1:13; 1Nya 4:43
[g]**14:49** 1Sam 31:2; 1Nya 8:33; Mwa 29:26; 1Sam 18:17-20
[h]**14:50** 2Sam 2:8; 3:6; 1Fal 2:5; 1Sam 10:14
[i]**14:51** 1Sam 9:1
[j]**14:52** 1Sam 8:11
[k]**15:1** 1Sam 9:16
[l]**15:2** Mwa 14:7; 1Sam 14:48; 2Sam 1; 8; Kut 17:8-14; Kum 25:17
[m]**15:3** Mwa 14:23; Yos 6:17; 1Sam 22:17; 22:19; 27:9; 28:8; Es 3:13; 9:5; Law 27:28; Kut 20:5; Isa 14:21; Mwa 3:17; Yos 7:24
[n]**15:4** Yos 15:24
[o]**15:6** Mwa 15:19; Hes 24:22; Amu 1:16; 1Sam 30:29; Mwa 18:25; 19:12; Mdo 2:40; Ufu 18:4; Kut 18:10; Hes 10:29

[7] [a]Ndipo Sauli akawashambulia Waamaleki
toka Havila mpaka Shuri, hadi mashariki
ya Misri. [8] [b]Akamchukua Agagi, mfalme
wa Waamaleki akiwa hai, nao watu wake
wote akawaangamiza kabisa kwa upanga.
[9] [c]Lakini Sauli na hilo jeshi wakamhifadhi
hai Agagi na kondoo na ng'ombe walio
wazuri, mafahali na wana-kondoo
walionona kila kitu kilichokuwa kizuri. Hivi
vitu hawakuwa radhi kuviangamiza kabisa,
bali kila kitu kilichodharauliwa na kilicho
dhaifu wakakiangamiza kabisa.

[10] Kisha neno la BWANA likamjia
Samweli kusema: [11] [d]"Ninasikitika
kwamba nimemfanya Sauli kuwa mfalme,
kwa sababu ameacha kunifuata mimi na
hakutimiza maagizo yangu." Samweli
akafadhaika, naye akamlilia BWANA usiku
ule wote.

[12] [e]Asubuhi na mapema Samweli
akaamka kwenda kukutana na Sauli, lakini
akaambiwa, "Sauli amekwenda Karmeli.
Huko amesimamisha mnara kwa heshima
yake mwenyewe naye ameendelea na
kuteremkia Gilgali."

[13] [f]Samweli alipomfikia, Sauli
akamwambia, "BWANA akubariki!
Nimetimiza yale BWANA aliniagiza."

[14] Lakini Samweli akasema, "Nini basi
huu mlio wa kondoo masikioni mwangu?
Huu mlio wa ng'ombe ninaousikia ni kitu
gani?"

[15] [g]Sauli akajibu, "Askari wamewaleta
kutoka kwa Waamaleki, waliwaacha wale
kondoo na ng'ombe wazuri ili kuwatoa
dhabihu kwa BWANA, Mungu wako, lakini
tuliwaangamiza kabisa wengine wote."

[16] Samweli akamwambia Sauli, "Ngoja!
Nami nitakuambia lile BWANA aliloniambia
usiku huu."

Sauli akajibu, "Niambie."

[17] [h]Samweli akamwambia, "Ingawa
zamani ulijiona mdogo machoni pako
mwenyewe, Je, hukuwa kiongozi wa kabila
za Israeli? BWANA alikutia mafuta kuwa
mfalme juu ya Israeli. [18] Naye akakutuma
kwa kazi maalum, akisema, 'Nenda
ukaangamize kabisa wale watu waovu,
wale Waamaleki, upigane nao vita mpaka
utakapowaangamiza kabisa.' [19] [i]Kwa nini
hukumtii BWANA? Kwa nini ulivamia nyara
na kufanya uovu machoni pa BWANA?"

[20] [j]Sauli akasema, "Lakini nilimtii BWANA.
Nilikamilisha ile kazi ambayo BWANA
alinituma. Niliwaangamiza Waamaleki
kabisa na kumleta Agagi mfalme wao.
[21] Askari walichukua kondoo na ng'ombe
kutoka kwenye nyara, zile ambazo ni nzuri
sana zimewekwa wakfu kwa Mungu, ili
zitolewe dhabihu kwa BWANA Mungu wako
huko Gilgali."

[22] [k]Lakini Samweli akajibu:

"Je, BWANA anafurahia sadaka za
kuteketezwa na dhabihu
kama vile kuitii sauti ya BWANA?
Kutii ni bora zaidi kuliko dhabihu,
nako kusikia ni bora
kuliko mafuta ya kondoo dume.
[23] [l]Kwa maana kuasi ni kama dhambi
ya uaguzi,
nao ukaidi ni kama uovu wa
kuabudu sanamu.
Kwa sababu umelikataa neno la
BWANA,
naye amekukataa wewe
kuendelea kuwa mfalme."

---

[a]**15:7** 1Sam 14:48; Mwa 16:7; 25:17-18; Kut 15:22
[b]**15:8** Kut 17:8-16; Hes 24:7; Yos 8:23; 1Fal 20:34; Es 3:1; 1Sam 30:1
[c]**15:9** Mit 15:27; 1Tim 6:10
[d]**15:11** Mwa 6:6; Kut 32:14; Yos 22:16; Ay 21:14; 34:27; Za 28:5; Isa 5:12; 53:6; Yer 48:10; Eze 18:24; 1Sam 8:6; Yos 22:16; 1Fal 9:6; Za 36:3; Sef 1:6; Mt 24:13
[e]**15:12** Yos 15:55; Hes 32:42
[f]**15:13** Mwa 14:19; Amu 17:2; Rut 3:2; Lk 8:11
[g]**15:15** Mwa 3:12; Mit 28:13
[h]**15:17** Kut 3:11; 1Sam 9:21
[i]**15:19** Mwa 14:23; 1Sam 14:32
[j]**15:20** 1Sam 28:18
[k]**15:22** Za 40:6-8; 51:16; Mit 21:3; Isa 1:11-15; Yer 7:22; Hos 6:6; Amo 5:25; Mik 6:6-8; Mk 12:33; Mt 12:7; Ebr 10:6; Kut 19:5; Mhu 5:1; Yer 7:23; Hos 6:6; Mt 5:24; 9:13
[l]**15:23** Kum 18:10; 1Sam 13:13

24 [a]Ndipo Sauli akamwambia Samweli,
“Nimetenda dhambi. Nimevunja amri ya
BWANA na maagizo yako. Niliwaogopa watu
na kwa hiyo nikafanya walivyotaka. 25 [b]Sasa
ninakusihi usamehe dhambi yangu, nawe
urudi pamoja nami, ili nipate kumwabudu
BWANA.”
26 [c]Lakini Samweli akamwambia, “Sitarudi
pamoja nawe. Umelikataa neno la BWANA,
naye BWANA amekukataa wewe, usiendelee
kuwa mfalme juu ya Israeli!”
27 [d]Samweli alipogeuka ili aondoke,
Sauli akang’ang’ania pindo la joho lake,
nalo likararuka. 28 [e]Samweli akamwambia,
“BWANA ameurarua ufalme wa Israeli
kutoka kwako leo, naye ameutia kwa
mmoja wa majirani zako, aliye bora kuliko
wewe. 29 [f]Yeye aliye Utukufu wa Israeli
hasemi uongo wala hana kigeugeu; kwa
kuwa yeye si mwanadamu, hata abadili
nia yake.”
30 [g]Sauli akajibu, “Nimetenda dhambi.
Lakini tafadhali niheshimu mbele ya wazee
wa watu wangu na mbele ya Israeli; rudi
pamoja nami, ili nipate kumwabudu BWANA
Mungu wako.” 31 Hivyo Samweli akarudi
pamoja na Sauli, naye Sauli akamwabudu
BWANA.
32 Ndipo Samweli akasema, “Niletee
Agagi mfalme wa Waamaleki.”
Agagi akaja kwake kwa ujasiri, akifikiri,
“Hakika uchungu wa mauti umepita.”
33 [h]Lakini Samweli akasema,

“Kama upanga wako ulivyofanya
wanawake
kufiwa na watoto wao,
ndivyo mama yako atakavyokuwa
hana mtoto miongoni mwa
wanawake.”

Naye Samweli akamuua Agagi mbele za
BWANA huko Gilgali.
34 [i]Kisha Samweli akaenda Rama, lakini
Sauli akapanda nyumbani kwake huko
Gibea ya Sauli. 35 [j]Hadi siku Samweli
alipofariki hakwenda kumwona Sauli tena,
ingawa Samweli alimwombolezea. Naye
BWANA alihuzunika kwamba alimfanya
Sauli kuwa mfalme juu ya Israeli.

### *Samweli Anamtia Daudi Mafuta*

16 [k]BWANA akamwambia Samweli,
“Utamlilia Sauli mpaka lini, maadamu
nimemkataa asiendelee kuwa mfalme juu
ya Israeli? Jaza pembe yako mafuta, ushike
njia uende; ninakutuma kwa Yese huko
Bethlehemu. Nimemchagua mmoja wa
wanawe kuwa mfalme.”
2 [l]Lakini Samweli akasema,
“Nitakwendaje? Sauli atasikia juu ya jambo
hili na ataniua.”
BWANA akamwambia, “Chukua mtamba
wa ng’ombe na useme, ‘Nimekuja kumtolea
BWANA dhabihu.’ 3 [m]Mwalike Yese aje
kwenye dhabihu, nami nitakuonyesha
utakalofanya. Utamtia mafuta kwa ajili
yangu yule nitakayekuonyesha.”
4 [n]Samweli akafanya kile BWANA
alichosema. Alipofika Bethlehemu, wazee
wa mji wakatetemeka walipomlaki.
Wakauliza, “Je, umekuja kwa amani?”
5 [o]Samweli akajibu, “Ndiyo, kwa amani;

[a]**15:24** Kut 9:27; Hes 22:24; Za 51:4; 1Sam 13:13; Mit 29:25; Isa 51:12-13; Yer 42:11; 2Sam 12:13; Mt 27:4; Ay 31:34; Mit 29:25; Ufu 21:8
[b]**15:25** Kut 10:17
[c]**15:26** Hes 15:31; 1Sam 13:14; 1Fal 14:10
[d]**15:27** 1Sam 28:14; 1Fal 11:11; 14:8; 2Fal 17:21
[e]**15:28** 1Sam 28:17; 13:14; 2Sam 6:21; 7:15; 1Fal 11:31
[f]**15:29** Tit 1:2; Hes 23:19; Ebr 7:21; 1Nya 29:11; Eze 24:14
[g]**15:30** Hes 22:34; Isa 29:13; Yn 12:43; 12:41-43; Rum 2:28-29
[h]**15:33** Es 9:7-10; Yer 18:21; Mwa 9:6; Kut 17:11; Amu 1:7; Yak 2:13; 1Fal 18:40
[i]**15:34** 1Sam 7:17; Amu 19:14; 1Sam 10:5; 11:4
[j]**15:35** 1Sam 19:24; 16:1; Mwa 6:6
[k]**16:1** 1Sam 8:6; 15:35; 13:14; 10:1; Rut 4:17; 2Sam 5:2; 7:8; 1Fal 8:16; 1Nya 12:23; Za 78:70; Mdo 13:22; 1Sam 9; 16
[l]**16:2** 1Sam 20:29
[m]**16:3** Kut 4:15; Kum 17:15; 1Sam 9:16
[n]**16:4** Mwa 48:7; Lk 2:4; 1Sam 21:1; 1Fal 2; 13; 2Fal 9:17; 2Sam 6:9; 1Fal 17:18; Hos 6:5; 11:10; Lk 18:11
[o]**16:5** Kut 19:10, 22

nimekuja kumtolea BWANA dhabihu.
Jiwekeni wakfu na mje kwenye dhabihu
pamoja nami.” Ndipo akamweka Yese
wakfu pamoja na wanawe na kuwaalika
kwenye dhabihu.
6 [a]Walipofika, Samweli akamwona Eliabu,
naye akafikiri, “Hakika mpakwa mafuta wa
BWANA anasimama hapa mbele za BWANA.”
7 [b]Lakini BWANA akamwambia Samweli,
“Usitazame sura yake wala kimo chake,
kwa kuwa nimemkataa. BWANA hatazami
katika vile vitu mwanadamu avitazamavyo.
Mwanadamu hutazama katika sura ya nje,
lakini BWANA hutazama moyoni.”
8 [c]Kisha Yese akamwita Abinadabu na
kumpitisha mbele ya Samweli. Lakini
Samweli akasema, “Hata huyu BWANA
hakumchagua.” 9 [d]Kisha Yese akampitisha
Shama, lakini Samweli akasema, “Wala
huyu BWANA hakumchagua.” 10 Yese
alikuwa na wana saba aliowapitisha mbele
ya Samweli, lakini Samweli akamwambia,
“BWANA hajawachagua hawa.” 11 [e]Hivyo
akamuuliza Yese, “Je, hawa ndio wana
pekee ulio nao?”

Yese akajibu, “Bado yuko mdogo kuliko
wote, lakini anachunga kondoo.”

Samweli akasema, “Tuma aitwe;
hatutaketi mpaka afike.”
12 [f]Basi akatuma aitwe naye akaletwa.
Alikuwa mwekundu, mwenye sura nzuri
na umbo la kupendeza.

Ndipo BWANA akasema, “Inuka na umtie
mafuta, huyu ndiye.”
13 [g]Basi Samweli akachukua ile pembe ya
mafuta na kumtia mafuta mbele ya ndugu
zake, kuanzia siku ile na kuendelea Roho
wa BWANA akaja juu ya Daudi kwa nguvu.
Kisha Samweli akaenda zake Rama.

*Daudi Katika Utumishi Kwa Sauli*

14 [h]Basi Roho wa BWANA alikuwa
ameondoka kwa Sauli, nayo roho mbaya
ikaachiwa nafasi na BWANA ili imtese.
15 Watumishi wa Sauli wakamwambia,
“Angalia, roho mbaya imeachiwa nafasi
na BWANA nayo inakutesa. 16 [i]Basi bwana
wetu na aamuru watumishi wake walioko
hapa kutafuta mtu ambaye anaweza kupiga
kinubi. Atakipiga kinubi wakati roho mbaya
iliyoachiwa nafasi na Mungu ikujiapo, nawe
utajisikia vizuri.”
17 Basi Sauli akawaambia watumishi
wake, “Mtafuteni mtu apigaye kinubi vizuri
mkamlete kwangu.”
18 [j]Mmoja wa watumishi wake akajibu,
“Nimemwona mwana wa Yese Mbethlehemu
ambaye anajua kupiga kinubi. Yeye ni
mtu hodari na shujaa wa vita. Ni mwenye
busara katika kunena, mtu mzuri wa umbo.
BWANA yu pamoja naye.”
19 [k]Ndipo Sauli akatuma wajumbe kwa
Yese na kumwambia, “Nitumie mwanao
Daudi, ambaye anachunga kondoo.” 20 [l]Kwa
hiyo Yese akamchukua punda aliyepakizwa
mikate, kiriba cha divai na mwana-mbuzi,
na kuvipeleka vitu hivyo kwa Sauli pamoja
na Daudi mwanawe.
21 [m]Daudi akafika kwa Sauli na kuingia
kwenye kazi yake. Sauli akampenda sana,
naye Daudi akawa mmoja wa wabeba
silaha wake. 22 Basi Sauli akatuma ujumbe
kwa Yese, akisema, “Mruhusu Daudi
abaki katika utumishi wangu, kwa kuwa
ninapendezwa naye.”
23 [n]Kila mara roho mbaya iliyoachiwa
nafasi na Mungu ilipomjia Sauli, Daudi
alichukua kinubi chake na kupiga. Ndipo
Sauli angetulizwa na kujisikia vizuri, nayo
ile roho mbaya ingemwacha.

---

[a]**16:6** 1Sam 17:13; 1Nya 2:13; 1Fal 12:26
[b]**16:7** Za 147:10; 1Sam 2:3; 2Sam 7:20; Za 44:21; 139:23; Ufu 2:23; Isa 55:8; 55:8; 2Kor 10:7; 1Fal 8:39; 1Nya 29:8; Yer 11:20; 17:10
[c]**16:8** 1Sam 17:13
[d]**16:9** 1Sam 17:13; 2Sam 13:3; 21:21
[e]**16:11** 1Sam 17:12; Mwa 37:2; 2Sam 7:8; Za 78:70
[f]**16:12** 1Sam 9:17; Mwa 39:6; 1Sam 17:42; Wim 5:10
[g]**16:13** 1Sam 2:35; 2Sam 22:51; 1Sam 18; 12; 11:6; Hes 27:18; Amu 11:29; 1Sam 6:9-10
[h]**16:14** Amu 16:20; 9:23; 1Sam 18; 10; 2Sam 7:15; 1Sam 19:9; Isa 19:14; Za 51:11
[i]**16:16** 1Sam 10:5-6; 2Nya 29:26-27; 2Fal 3:15; Za 49:4
[j]**16:18** Rut 4:17; 2Sam 17:8; Mwa 39:2; 1Sam 17:37; 20:13; 1Nya 22:11; Mt 1:23
[k]**16:19** 1Sam 17:15
[l]**16:20** Mwa 32:13; 1Sam 10:4; Mit 18:16
[m]**16:21** Mwa 41:46; Mit 22:29; 1Fal 10:8; Mit 22:29
[n]**16:23** Amu 9:23

### *Daudi Na Goliathi*

17 [a]Wakati huu Wafilisti wakakusanya
majeshi yao kwa ajili ya vita, nao
wakakusanyika huko Soko katika Yuda.
Wakapiga kambi huko Efes-Damimu, kati
ya Soko na Azeka. 2 [b]Sauli na Waisraeli
wakakusanyika na kupiga kambi katika
Bonde la Ela na kupanga jeshi ili kupigana
vita na Wafilisti. 3 Wafilisti wakawa katika
kilima kimoja na Waisraeli katika kilima
kingine, hilo bonde likiwa kati yao.
4 [c]Shujaa aliyeitwa Goliathi, aliyetoka
Gathi, akajitokeza kutoka kambi ya
Wafilisti. Alikuwa na urefu dhiraa sita na
shibiri moja.[d] 5 Alikuwa na chapeo ya shaba
kichwani mwake, na alivaa dirii ya shaba
kifuani mwake yenye uzito wa shekeli elfu
tano.[e] 6 [f]Miguuni mwake alivaa mabamba
ya shaba, na alikuwa na mkuki wa shaba
mgongoni mwake. 7 [g]Mpini wa huo mkuki
ulikuwa kama mti wa mfumaji, na ncha ya
chuma yake ilikuwa na uzito wa shekeli
mia sita.[h] Mbeba ngao wake alitangulia
mbele yake.
8 [i]Goliathi alisimama na kuwapigia kelele
majeshi ya Israeli, akisema, “Kwa nini
mmetoka kupanga vita? Je, mimi si Mfilisti,
na ninyi ni watumishi wa Sauli? Chagueni
mtu na anishukie mimi. 9 [j]Kama anaweza
kupigana nami na kuniua, tutakuwa chini
yenu; lakini kama nikimshinda na kumuua,
ninyi mtakuwa chini yetu na mtatutumikia.”
10 [k]Kisha yule Mfilisti akasema, “Siku hii ya
leo nayatukana majeshi ya Israeli! Nipeni
mtu tupigane.” 11 Kwa kusikia maneno
ya Wafilisti, Sauli na Waisraeli wote
wakafadhaika na kuogopa.
12 [l]Basi Daudi alikuwa mwana wa
Mwefrathi jina lake Yese aliyekuwa ametoka
Bethlehemu ya Yuda. Yese alikuwa na wana
wanane, naye wakati wa Sauli alikuwa mzee
tena wa umri mkubwa. 13 [m]Wana wakubwa
watatu wa Yese walikuwa wamefuatana na
Sauli vitani: Mzaliwa wa kwanza alikuwa
Eliabu, wa pili Abinadabu, na wa tatu
Shama. 14 Daudi ndiye alikuwa mdogo wa
wote. Hao wakubwa watatu wakamfuata
Sauli, 15 [n]lakini Daudi alikuwa akienda kwa
Sauli na kurudi ili kuchunga kondoo wa
baba yake huko Bethlehemu.
16 Kwa siku arobaini huyo Mfilisti alikuwa
akija mbele kila siku asubuhi na jioni na
kujionyesha.
17 [o]Wakati huo Yese akamwambia
mwanawe Daudi, “Chukua hii efa[p] ya bisi
na hii mikate kumi kwa ajili ya ndugu
zako uwapelekee upesi kambini mwao.
18 [q]Chukua pamoja na hizi jibini kumi kwa
jemadari wa kikosi chao. Ujue hali ya ndugu
zako na unilete taarifa za uhakika kutoka
kwao. 19 Wao wako pamoja na Sauli na watu
wote wa Israeli huko kwenye Bonde la Ela,
wakipigana na Wafilisti.”
20 Asubuhi na mapema Daudi akaondoka,
akaliacha kundi la kondoo pamoja na
mchungaji, akapakia vitu vile na kuondoka,
kama vile Yese alivyokuwa amemwagiza.
Akafika kambini wakati jeshi lilikuwa
likitoka kwenda kwenye sehemu yake ya
kupigania, huku wakipiga kelele za vita.
21 Israeli na Wafilisti walikuwa wakipanga
safu zao wakitazamana. 22 [r]Daudi
akaacha vile vitu vyake kwa mtunza
vifaa, akakimbilia katika safu za vita na
kuwasalimu ndugu zake. 23 [s]Alipokuwa
akisema nao, Goliathi, yule Mfilisti shujaa
kutoka Gathi, akajitokeza mbele ya safu

[a]**17:1** 1Sam 13:5; Yos 15:35; 2Nya 28:18; Yos 10:10, 11
[b]**17:2** 1Sam 21:9
[c]**17:4** 1Sam 21:9; Yos 11:21-22; 2Sam 21:19; 1Nya 20:5; 8:13; 18:1; 2Nya 26:6; Amo 6:2
[d]4 Dhiraa sita na shibiri moja ni sawa na mita 3, au futi 9 na inchi 8.
[e]5 Shekeli 15,000 ni sawa na kilo 50.
[f]**17:6** 1Sam 18:10
[g]**17:7** 2Sam 21:19; 1Nya 11:23; 20:5
[h]7 Shekeli 600 ni sawa na kilo 7.
[i]**17:8** 2Sam 2:12-17; 1Sam 8:17; 1Nya 21:3
[j]**17:9** 1Sam 11:1
[k]**17:10** 2Sam 21:21; Hes 23:7-8; Neh 2:19
[l]**17:12** Mwa 35:16; 48:7; Za 132:6; Rut 4:17, 22; 1Sam 16; 11; Mwa 35:19; 1Sam 16:10, 11; 1Nya 2:13
[m]**17:13** 1Sam 16:6-9; 1Nya 2:13
[n]**17:15** 1Sam 16:19; Mwa 37:2
[o]**17:17** Mwa 37:14
[p]17 Efa moja ni sawa na kilo 22.
[q]**17:18** Law 19:36; 23:14; 1Sam 25:18
[r]**17:22** Mwa 37:14
[s]**17:23** Mwa 43:27; Amu 18:15

zake na kupiga ile kelele yake ya kawaida
ya matukano, naye Daudi akayasikia.
24 Waisraeli walipomwona yule mtu, wote
wakamkimbia kwa woga mkuu.
25 [a]Basi Waisraeli walikuwa wakisema,
“Je, mnaona jinsi mtu huyu anavyoendelea
kujitokeza. Hujitokeza ili kutukana Israeli.
Mfalme atatoa utajiri mwingi kwa yule mtu
atakayemuua. Pia atamwoza binti yake na
atasamehe jamaa ya baba yake kulipa kodi
katika Israeli.”
26 [b]Daudi akauliza watu waliokuwa
wamesimama karibu naye, “Je, atafanyiwa
nini mtu atakayemuua huyu Mfilisti na
kuondoa aibu hii katika Israeli? Ni nani
huyu Mfilisti asiyetahiriwa hata atukane
majeshi ya Mungu aliye hai?”
27 Wakarudia yale yaliyokuwa
yamesemwa na kumwambia kuwa,
“Hili ndilo atakalotendewa mtu yule
atakayemuua.”
28 [c]Eliabu nduguye mkubwa Daudi
alipomsikia akizungumza na watu hasira
ikawaka juu yake akamuuliza, “Kwa nini
umeteremka kuja hapa? Nao wale kondoo
wachache kule nyikani umewaacha na
nani? Ninajua jinsi ulivyo na kiburi na jinsi
moyo wako ulivyo mwovu; umekuja hapa
kutazama vita tu.”
29 [d]Daudi akasema, “Sasa nimefanya
nini? Je, siwezi hata kuongea.” 30 Daudi
akamgeukia mtu mwingine na kumuuliza
jambo lilo hilo, nao watu wakamjibu vilevile
kama mwanzo. 31 Lile Daudi alilosema
likasikiwa na kuelezwa kwa Sauli, naye
Sauli akatuma aitwe.
32 [e]Daudi akamwambia Sauli, “Mtu yeyote
asife moyo kwa habari ya huyu Mfilisti;
mtumishi wako atakwenda kupigana naye.”
33 [f]Sauli akamjibu Daudi, “Wewe
hutaweza kwenda kupigana dhidi ya huyu
Mfilisti; wewe ni kijana tu, naye amekuwa
mtu wa vita tangu ujana wake.”
34 [g]Lakini Daudi akamwambia Sauli,
“Mtumishi wako amekuwa akichunga
kondoo wa baba yake. Wakati simba
au dubu alikuja na kuchukua kondoo
kutoka kundi, 35 [h]nilifuatia, nikampiga na
nikampokonya kondoo kwenye kinywa
chake. Aliponigeukia, nilimkamata nywele
zake, nikampiga na kumuua. 36 [i]Mtumishi
wako ameshaua simba na dubu pia; huyu
Mfilisti asiyetahiriwa atakuwa kama mmoja
wa hao, kwa sababu ameyatukana majeshi
ya Mungu aliye hai. 37 [j]BWANA ambaye
aliniokoa toka katika makucha ya simba na
makucha ya dubu ataniokoa kutoka mikono
ya huyu Mfilisti.”
Sauli akamwambia Daudi, “Nenda, naye
BWANA na awe pamoja nawe.”
38 [k]Ndipo Sauli akamvika Daudi silaha
zake mwenyewe za vita. Akamvika dirii na
chapeo ya shaba kichwani mwake. 39 Daudi
akajifunga upanga juu ya hayo mavazi na
kujaribu kutembea kwa sababu alikuwa
hana uzoefu navyo.
Daudi akamwambia Sauli, “Siwezi
kwenda nikiwa nimevaa hivi, kwa sababu
sina uzoefu navyo.” Hivyo akavivua. 40 Kisha
akachukua fimbo yake mkononi, akachagua
mawe laini matano kutoka kwenye kijito,
akayaweka kwenye kifuko ndani ya mfuko
wake wa kichungaji, akiwa na kombeo yake
mkononi mwake, akamkaribia yule Mfilisti.
41 Wakati ule ule, yule Mfilisti, akiwa
na mbeba ngao wake mbele yake,
akaendelea kujongea karibu na Daudi.
42 [l]Mfilisti akamwangalia Daudi kote na
kumwona kuwa ni kijana tu, mwekundu
na mzuri wa kupendeza, naye akamdharau.

[a]**17:25** Yos 1:11; 15:16
[b]**17:26** 1Sam 18:17; 8:15; Yos 15:16; Kum 5:26; Yer 10:10
[c]**17:28** Mwa 27:41; Mit 18:19; Mwa 37:8, 11; Mt 10:38; Mwa 37:4; Mhu 4:4; Mk 3:21
[d]**17:29** Mit 15:1
[e]**17:32** Kum 20:3; Za 18:45; Isa 7:4; Yer 4:9; 38:4; Dan 11:30; Hes 13:30; 14:9; Ebr 12:12; Isa 30:3
[f]**17:33** Hes 13:31; Kum 9:2
[g]**17:34** Ay 10:16; Isa 31:4; Yer 49:19; Hos 13:8; Amo 3:12
[h]**17:35** Amu 14:6
[i]**17:36** 1Nya 11:22
[j]**17:37** 2Kor 1:10; 2Tim 4:17; 1Sam 16:18; 18:12; 1Nya 22:11, 16; 1Sam 7:12; Za 18:16, 17
[k]**17:38** Mwa 41:42
[l]**17:42** 1Sam 16:12; Za 123:3-4; Mit 16:18; 1Kor 1:27, 28

43 [a]Akamwambia Daudi, “Je, mimi ni mbwa,
hata unanijia na fimbo?” Yule Mfilisti
akamlaani Daudi kwa miungu yake. 44 [b]Tena
Mfilisti akamwambia, “Njoo hapa, nami
nitawapa ndege wa angani na wanyama
wa mwituni nyama yako.”
45 [c]Daudi akamwambia yule Mfilisti.
“Wewe unanijia na upanga, mkuki na fumo,
lakini mimi ninakujia kwa jina la Bwana
Mwenye Nguvu Zote, Mungu wa majeshi ya
Israeli, ambaye wewe umemtukana. 46 [d]Siku
hii leo Bwana atakutia mkononi mwangu,
nami nitakupiga na kukukata kichwa chako.
Leo nitawapa ndege wa angani na wanyama
wa nchi mizoga ya jeshi la Wafilisti, nayo
dunia yote itajua kuwa yuko Mungu katika
Israeli. 47 [e]Wale wote waliokusanyika hapa
watajua kuwa Bwana haokoi kwa upanga
wala kwa mkuki; kwa kuwa vita ni vya
Bwana, naye atawatia wote mikononi
mwetu.”
48 Yule Mfilisti aliposogea karibu ili
kumshambulia, Daudi akaenda mbio
kuelekea safu ya vita kukutana naye.
49 Daudi akatia mkono wake mfukoni na
kuchukua jiwe, akalirusha kwa kombeo,
nalo likampiga yule Mfilisti kwenye paji la
uso. Lile jiwe likaingia kipajini mwa uso,
akaanguka chini kifudifudi.
50 [f]Basi Daudi akamshinda huyo Mfilisti
kwa kombeo na jiwe; bila kuwa na upanga
mikononi mwake akampiga huyo Mfilisti
na kumuua.
51 [g]Daudi akakimbia na kusimama juu
yake. Akaushika upanga wa huyo Mfilisti
na kuuvuta toka kwenye ala yake. Baada
ya kumuua, akakata kichwa chake kwa ule
upanga.
Wafilisti walipoona kuwa shujaa wao
amekufa, wakageuka na kukimbia. 52 [h]Ndipo
watu wa Israeli na Yuda wakainuka kwenda
mbele wakipiga kelele na kufuatia Wafilisti
mpaka kwenye ingilio la Gathi kwenye
malango ya Ekroni. Maiti zao zilitawanyika
kando ya barabara ya Shaaraimu hadi Gathi
na Ekroni. 53 Waisraeli waliporudi kutoka
kuwafukuza Wafilisti, waliteka nyara kutoka
kambi yao. 54 Daudi akachukua kichwa cha
yule Mfilisti na kukileta Yerusalemu, naye
akaweka silaha za huyo Mfilisti katika hema
lake mwenyewe.
55 [i]Sauli alipomwona Daudi anakwenda
kukabiliana na huyo Mfilisti, alimwambia
Abneri, jemadari wa jeshi, “Abneri, yule
kijana ni mwana wa nani?”
Abneri akajibu, “Hakika kama uishivyo,
ee mfalme, mimi sifahamu.”
56 Mfalme akasema, “Uliza huyu kijana
ni mwana wa nani.”
57 Mara Daudi aliporudi kutoka kumuua
huyo Mfilisti, Abneri akamchukua na
kumleta mbele ya Sauli. Daudi alikuwa
bado anakishikilia kichwa cha yule Mfilisti.
58 [j]Sauli akamuuliza, “Kijana, wewe ni
mwana wa nani?”
Daudi akasema, “Mimi ni mwana wa
mtumishi wako Yese wa Bethlehemu.”

### *Sauli Amwonea Daudi Wivu*

18 [k]Baada ya Daudi kumaliza kuongea na
Sauli, roho ya Yonathani ikaambatana
na roho ya Daudi, naye akampenda
kama nafsi yake mwenyewe. 2 [l]Kuanzia
siku ile Sauli akamchukua Daudi naye
hakumruhusu kurudi nyumbani kwa baba
yake. 3 [m]Yonathani akafanya agano na
Daudi kwa sababu alimpenda kama nafsi

[a]**17:43** 1Sam 24:14; 2Sam 3:8; 9:8; 2Fal 8:13
[b]**17:44** Mwa 40:19; Ufu 19:7; 2Sam 21:10; Yer 34:20; 1Fal 20:10-11
[c]**17:45** Kum 20:1; 2Nya 13:12; 14:11; 32:8; Za 20:7-8; 124:8; Ebr 11:32-34; 2Sam 22:33, 35; 2Nya 32:8; Za 124:8; 125:1; Mit 18:10; Flp 4:13
[d]**17:46** 1Sam 14:12; Kum 28:26; Yos 4; 24; Isa 11:9; 1Fal 18:36; 2Fal 5:8; 19:19; Isa 37:20; Za 44:6-7; Zek 4:6
[e]**17:47** 1Sam 25:29; 2Sam 23:21; Za 44:6, 7; Hos 1:7; Zek 4:6; 2Nya 20:15
[f]**17:50** Ebr 11:34; 1Sam 21:9; 22:10; Amu 3:31; 15:15; 2Sam 23:21
[g]**17:51** Ebr 11:34
[h]**17:52** Yos 15:11; 15:36
[i]**17:55** 1Sam 16:21; 26:5
[j]**17:58** Rut 4:17
[k]**18:1** 1Sam 19:1; 20:16; 31:2; 2Sam 4:4; 1:26; Mwa 44:30; Kol 2:2; Kum 13:6; 1Sam 20:17; Mit 18:24; Yn 15:17-19; 1Yn 3:12-14
[l]**18:2** 1Sam 8:11; 14:52; 17:15
[m]**18:3** 1Sam 20:8, 16, 17, 42; 22:8; 23:18; 24:21; 2Sam 21:7

yake mwenyewe. 4 [a]Yonathani akavua joho alilokuwa amevaa na kumpa Daudi, pamoja na koti lake, silaha zake, hata pamoja na upanga wake, upinde wake na mshipi wake.

5 [b]Lolote Sauli alilomtuma Daudi kufanya, alitenda kwa hekima, hata Sauli akampa cheo cha juu katika jeshi. Jambo hili likawapendeza watu wote, hata maafisa wa Sauli pia.

6 [c]Watu walipokuwa wanarudi nyumbani baada ya Daudi kumuua yule Mfilisti, wanawake wakaja kutoka pande zote za miji ya Israeli kumlaki Mfalme Sauli kwa kuimba na kucheza, kwa nyimbo za furaha na kwa matari na zeze.

7 [d]Walipokuwa wanacheza, wakaimba:

“Sauli amewaua elfu zake,
  naye Daudi makumi elfu yake.”

8 [e]Sauli akakasirika sana; sehemu hii ya kurudia rudia ya wimbo huu ilimkasirisha sana. Akafikiri kuwa, “Wamempa Daudi makumi elfu, lakini mimi wamenipa elfu tu. Apate nini zaidi isipokuwa ufalme?” 9 [f]Kuanzia wakati ule na kuendelea Sauli akawa na jicho la wivu juu ya Daudi.

10 [g]Kesho yake roho mbaya iliyoachiwa nafasi na Mungu ikaja kwa nguvu juu ya Sauli. Alikuwa akitabiri nyumbani mwake, wakati Daudi alikuwa akipiga kinubi, kama alivyozoea. Sauli alikuwa na mkuki mkononi mwake; 11 [h]akautupa kwa nguvu, akijiambia mwenyewe, “Nitamchoma kwa mkuki abaki hapo ukutani.” Lakini Daudi akamkwepa mara mbili.

12 [i]Sauli akamwogopa Daudi, kwa sababu Bwana alikuwa pamoja na Daudi, lakini alikuwa amemwacha yeye. 13 [j]Kwa hiyo Sauli akamwondoa Daudi mbele yake na kumpa kuwa kiongozi wa watu elfu moja, naye Daudi akatoka na kuingia akiongoza vikosi katika vita. 14 [k]Katika kila kitu alichofanya, Daudi alipata mafanikio makubwa, kwa sababu Bwana alikuwa pamoja naye. 15 Sauli alipoona jinsi alivyokuwa akifanikiwa, akamwogopa. 16 [l]Lakini Israeli wote na Yuda walimpenda Daudi, kwa sababu ndiye alikuwa akiwaongoza katika vita vyao.

17 [m]Sauli akamwambia Daudi, “Huyu hapa binti yangu mkubwa Merabu. Nitakupa umwoe, endapo tu utanitumikia kwa ushujaa na kupigana vita vya Bwana.” Kwa maana Sauli alisema moyoni mwake, “Sitainua mkono wangu dhidi yake. Acha mkono wa Wafilisti uwe juu yake.”

18 [n]Lakini Daudi akamwambia Sauli, “Mimi ni nani, nayo jamaa yangu ni nini au ukoo wa baba yangu katika Israeli, kwamba mimi niwe mkwewe mfalme?” 19 [o]Basi ulipofika wakati wa Daudi kupewa Merabu, binti Sauli, huyo binti aliozwa kwa Adrieli, Mmeholathi.

20 [p]Basi Mikali binti Sauli alimpenda Daudi, nao walipomwambia Sauli juu ya jambo hili, likampendeza. 21 [q]Sauli akawaza, “Nitampa Daudi binti yangu, ili apate kuwa mtego kwake, ili kwamba mkono wa Wafilisti upate kuwa juu yake.” Hivyo Sauli akamwambia Daudi, “Sasa unayo nafasi ya pili ya kuwa mkwe wangu.”

22 Ndipo Sauli akawaagiza watumishi wake, akisema, “Zungumzeni na Daudi kwa siri na kumwambia, ‘Tazama, mfalme amependezwa nawe, nao watumishi wake wote wanakupenda. Basi na uwe mkwewe mfalme.’ ”

[a]**18:4** Mwa 41:42; 2Sam 18:11
[b]**18:5** 2Sam 5:2
[c]**18:6** Kut 15:20; 2Sam 1:20; Za 68:25; Amu 11:34; Yer 31:4
[d]**18:7** Kut 15:21; 1Sam 21:11; 29:5; 2Sam 18:3; Amu 5:3; 2Nya 5:13; Za 24:1-10; Isa 5:1
[e]**18:8** 1Sam 13:14; 15:8; Mhu 4:4
[f]**18:9** Mwa 4:5; 31:2, 5; Mt 20:15; Lk 15:28
[g]**18:10** Amu 9:23; 1Sam 16:14; 10:5; 16:21; 19:7; 17; 6; 1Fal 18:29; Mdo 16:16
[h]**18:11** 1Sam 20:7, 33; 19:10; Za 132:1
[i]**18:12** 1Sam 16:13; Yos 1:5; 1Sam 17:37; 20:13; 1Nya 22:11; Amu 16:20
[j]**18:13** Hes 27:17; 2Sam 5:2
[k]**18:14** Mwa 39:2, 3; Hes 14:43; 2Sam 7:9; Yos 6:27
[l]**18:16** 2Sam 5:2
[m]**18:17** 1Sam 17:25; Mwa 29:26; Hes 21:14; 1Sam 20:33; 25:28
[n]**18:18** Kut 3:11; 1Sam 9:21; 2Sam 7:18; Rut 2:10; Mit 15:33
[o]**18:19** 2Sam 21:8; Amu 7:22
[p]**18:20** Mwa 29:26
[q]**18:21** Kut 10:7; 7:16; Za 7:14-16; Mit 26:24-26; Yer 5:26; 9:8

23 Watumishi wa Sauli wakarudia hayo
maneno kwa Daudi. Lakini Daudi akasema,
“Je, mnafikiri ni jambo dogo kuwa mkwewe
mfalme? Mimi ni mtu maskini tu, na
nisiyejulikana sana.”
24 Watumishi wa Sauli walipomweleza
yale Daudi aliyoyasema, 25 [a]Sauli akajibu,
“Mwambieni Daudi, ‘Mfalme hataki zawadi
nyingine kuwa mahari isipokuwa magovi
100 ya Wafilisti, ili kulipiza kisasi juu ya
adui zake.’ ” Mawazo ya Sauli yalikuwa
Daudi akaanguke mikononi mwa Wafilisti.
26 Watumishi walipomwambia Daudi
mambo haya, ikampendeza kuwa mkwewe
mfalme. Basi kabla siku iliyopangwa
haijafika, 27 [b]Daudi na watu wake walitoka
na kuwaua Wafilisti mia mbili. Akayaleta
magovi yao na kupeleka hesabu kamilifu
kwa mfalme, ili kwamba apate kuwa
mkwewe mfalme. Ndipo Sauli akamwoza
Daudi Mikali binti yake.
28 Sauli alipotambua kuwa Bwana
alikuwa pamoja na Daudi na kwamba
Mikali binti yake anampenda Daudi,
29 [c]Sauli akazidi kumwogopa Daudi, naye
Sauli akabaki kuwa adui yake siku zote za
maisha yake.
30 [d]Majemadari wa jeshi la Wafilisti
waliendelea kupigana vita na kadiri
walivyoendelea kupigana, Daudi akazidi
kutenda kwa hekima kuliko maafisa wengine
wa Sauli, nalo jina lake likajulikana sana.

*Sauli Ajaribu Kumuua Daudi*

19 [e]Sauli akamwambia mwanawe
Yonathani na watumishi wake
wote wamuue Daudi. Lakini Yonathani
mwana wa Sauli alimpenda sana Daudi.
2 [f]Yonathani akamwonya Daudi, akisema,
“Baba yangu Sauli anatafuta nafasi ya
kukuua. Ujilinde kesho asubuhi, nenda
mahali pa siri na ukae huko. 3 [g]Nitatoka
na kukaa na baba yangu shambani mahali
uliko. Nitazungumza naye juu yako, nami
nitakueleza nitakachogundua.”
4 [h]Yonathani akanena mema juu ya Daudi
kwa Sauli baba yake na kumwambia,
“Mfalme asitende mabaya kwa mtumishi
wake Daudi; hajakukosea, aliyoyafanya
yamekuwa ya faida sana kwako.
5 [i]Alihatarisha maisha yake alipomuua yule
Mfilisti. Bwana akajipatia ushindi mkubwa
kwa ajili ya Israeli wote, nawe uliuona na
ukafurahi. Kwa nini basi utende mabaya
kwa mtu asiye na hatia kama Daudi kwa
kumuua bila sababu?”
6 Sauli akamsikiliza Yonathani na kuapa
hivi: “Hakika kama Bwana aishivyo, Daudi
hatauawa.”
7 [j]Basi Yonathani akamwita Daudi na
kumweleza mazungumzo yote. Akamleta
kwa Sauli, naye Daudi akawa pamoja na
Sauli kama kwanza.
8 Vita vilitokea tena, naye Daudi akatoka
na kupigana na Wafilisti. Akawapiga kwa
nguvu nyingi hata wakakimbia mbele yake.
9 [k]Lakini roho mbaya iliyoachiwa nafasi
na Bwana ikaja juu ya Sauli alipokuwa
ameketi katika nyumba yake akiwa na
mkuki mkononi mwake. Daudi alipokuwa
anampigia kinubi, 10 [l]Sauli akajaribu
kumchomea Daudi ukutani kwa huo mkuki
wake, lakini Daudi akauhepa huo mkuki wa
Sauli ukakita ukutani. Usiku ule ule Daudi
akakimbia na kuokoka.
11 [m]Sauli akatuma watu nyumbani mwa
Daudi wailinde hiyo nyumba na kumuua
asubuhi. Lakini Mikali, mkewe Daudi,
akamwonya akisema, “Kama hukukimbia
kuokoa maisha yako usiku huu, kesho yake

---

[a]**18:25** Mwa 34:12; Za 8:2; 44:16; Yer 20:10; Kut 22:17
[b]**18:27** 2Sam 3:14; 6:16
[c]**18:29** 1Sam 18:20; Mhu 4:4; Yak 2:13
[d]**18:30** 1Sam 11:1; Lk 21:15
[e]**19:1** 1Sam 18:1-9; Mit 27:4
[f]**19:2** Mdo 23:16
[g]**19:3** 1Sam 20:12
[h]**19:4** 1Sam 20:32; 22:14; Mit 31:8-9; Yer 18:20; 1Sam 25:21; Mit 17:13; Mwa 42:22; 1Nya 6:22; Za 35:12; 109:5; Yer 18:20; 1Kor 8:12; 1Yn 3:15
[i]**19:5** Amu 9:17; 1Sam 11:13; Mwa 31:36; Kum 19:10-13; 1Sam 17:49-50; 1Nya 11:14; Mt 27:4; Za 119:109; Mt 27:14
[j]**19:7** 1Sam 16:21; 18:10
[k]**19:9** Amu 9:23; 1Sam 10:5; 16:14
[l]**19:10** 1Sam 18:11; Ay 5:2; Za 5:6; Mit 1:16; 29:10
[m]**19:11** Za 59; Amu 16:2

utauawa.” 12 [a]Basi Mikali akamteremsha
Daudi kupitia dirishani, naye akakimbia
na kuokoka. 13 [b]Kisha Mikali akachukua
kinyago, akakilaza kitandani, akakifunika
kwa vazi na kukiwekea singa za mbuzi
kichwani.
14 [c]Sauli alipotuma watu kumkamata
Daudi, Mikali akasema, “Yeye ni mgonjwa.”
15 Kisha Sauli akatuma watu tena
kumwona Daudi naye akawaambia, “Mleteni
kwangu juu ya kitanda chake ili nipate
kumuua.” 16 Lakini wale watu walipoingia,
kumbe ni kinyago tu kilichokuwa kitandani
na kwenye kichwa kulikuwepo na singa
za mbuzi.
17 [d]Sauli akamwambia Mikali, “Kwa nini
umenidanganya mimi hivi na kumwacha
adui yangu aende zake ili apate kuokoka?”
Mikali akamwambia, “Yeye aliniambia,
‘Niache niende zangu. Kwa nini nikuue?’ ”
18 [e]Daudi alipokuwa amekimbia na
kuokoka, alimwendea Samweli huko Rama
na kumwambia yale yote Sauli alimfanyia.
Ndipo Daudi na Samweli wakaenda Nayothi
kukaa huko. 19 Habari zikamfikia Sauli
kusema: “Daudi yuko Nayothi huko Rama.”
20 [f]Basi Sauli akatuma watu kumkamata
Daudi, lakini walipoona kundi la manabii
wakitoa unabii, wakiwa pamoja na Samweli
akiwa amesimama hapo kama kiongozi
wao, Roho wa Mungu akaja juu ya watu
wa Sauli, nao pia wakatoa unabii. 21 Sauli
akaelezwa juu ya hilo, naye akapeleka
watu wengine zaidi, nao wakatoa unabii
pia. Sauli akatuma watu mara ya tatu, nao
pia wakatoa unabii. 22 Mwishowe, yeye
mwenyewe akaondoka kwenda Rama na
kwenda hadi kwenye kile kisima kikubwa
kilichoko huko Seku. Naye akauliza, “Wako
wapi Samweli na Daudi?”
Wakasema, “Wako Nayothi huko Rama.”
23 [g]Hivyo Sauli akaenda Nayothi huko
Rama. Lakini Roho wa Mungu akaja juu
yake hata yeye, akawa anatembea huku
anatoa unabii hadi akafika Nayothi.
24 [h]Akavua majoho yake na pia akatoa
unabii mbele ya Samweli. Akalala hali
hiyo ule mchana kutwa na usiku kucha.
Hii ndiyo sababu watu husema, “Je, Sauli
pia yumo miongoni mwa manabii?”

*Daudi Na Yonathani*

20 [i]Kisha Daudi akakimbia kutoka Nayothi
huko Rama akamwendea Yonathani na
kumuuliza, “Kwani nimefanya nini? Kosa
langu ni nini? Nimemkosea baba yako
kwa jinsi gani, hata kwamba anajaribu
kuuondoa uhai wangu?”
2 [j]Yonathani akajibu, “La hasha!
Hutakufa! Tazama, baba yangu hafanyi
kitu chochote, kikubwa au kidogo, bila
kuniambia mimi. Kwa nini anifiche hili?
Sivyo ilivyo!”
3 [k]Lakini Daudi akaapa na kusema, “Baba
yako anajua kabisa kwamba nimepata
kibali mbele yako, naye amesema moyoni
mwake, ‘Yonathani sharti asilijue hili, la
sivyo atahuzunika.’ Lakini kweli kama
BWANA aishivyo na kama uishivyo, kuna
hatua moja tu kati yangu na mauti.”
4 Yonathani akamwambia Daudi,
“Chochote unachotaka nifanye,
nitakufanyia.”
5 [l]Basi Daudi akamwambia, “Angalia,
kesho ni sikukuu ya Mwezi Mwandamo,
nami inanipasa kula chakula pamoja na
mfalme; lakini niache niende kujificha
shambani mpaka kesho kutwa. 6 [m]Kama

[a]**19:12** Yos 2:15; Mdo 9:25; 2Kor 11:33
[b]**19:13** Mwa 31:19; Amu 17:5
[c]**19:14** Kum 1:19; Yos 2:4
[d]**19:17** 2Sam 2:22
[e]**19:18** 1Sam 7:17; Mit 17:17; Mal 2:7
[f]**19:20** Hes 11:25-29; 1Sam 10:5; Yoe 2:28; Yn 7:32, 45; 1Kor 14:3, 24, 25
[g]**19:23** 1Sam 10:13; Mwa 31:24; Hes 23:5; 24:2; Mit 21:1; Dan 4:35; Mt 7:22; Yn 11:51; 1Kor 13:2
[h]**19:24** 2Sam 6:20; Isa 20:2; 1Sam 15:35; 10:11; Mik 1:8; Mdo 9:21
[i]**20:1** 1Sam 24:9; 22:23; 23:15; 24:11; 25:29; Za 40:14; 54:3; 63:9; 70:2
[j]**20:2** Mwa 44:7; Yos 22:29
[k]**20:3** Kum 6:13
[l]**20:5** Hes 10:10; 25:11; 1Sam 9:12; 2Fal 4:23; 1Nya 23:31; 2Nya 2:4; Ezr 3:5; Neh 10:33; Za 81:3; Isa 1:13; Eze 45:17; 46:6; Za 55:13; Yn 8:59
[m]**20:6** 1Sam 17:58; 1:3; 16:4; 9:12

baba yako akiona ya kuwa sipo, mwambie,
‘Daudi aliniomba sana ruhusa kuwahi
Bethlehemu, mji wake wa nyumbani, kwa
sababu dhabihu ya mwaka inafanywa huko
kwa ajili ya ukoo wake wote.’ 7 [a]Kama
akisema, ‘Ni vyema sana,’ basi mtumishi
wako yu salama. Lakini kama akikasirika,
unaweza kuwa na hakika kwamba
anakusudia kunidhuru. 8 [b]Lakini kwa habari
yako wewe, mtende wema mtumishi wako,
kwa sababu mmeingia kwenye agano
pamoja naye mbele za Bwana. Kama nina
hatia, basi niue wewe mwenyewe! Kwa nini
unikabidhi kwa baba yako?”

9 Yonathani akasema, “La hasha! Kama
ningekuwa na kidokezo kidogo kwamba
baba yangu amekusudia kukudhuru wewe,
je, nisingekuambia?”

10 Daudi akamuuliza, “Je, nani
atakayeniambia kama baba yako atakujibu
kwa ukali?”

11 Yonathani akamwambia, “Njoo, twende
shambani.” Basi wakaenda huko pamoja.

12 [c]Kisha Yonathani akamwambia
Daudi, “Ninakuahidi kwa jina la Bwana,
Mungu wa Israeli, hakika nitamchunguza
baba yangu wakati kama huu kesho
kutwa! Kama ameweka utaratibu wa
kufaa kukuhusu wewe, je, sitakutumia
ujumbe na kukufahamisha? 13 [d]Lakini
ikiwa baba yangu amenuia kukudhuru,
Bwana na anishughulikie kwa ukali,
iwapo sitakufahamisha na kukuaga uende
salama. Bwana na awe pamoja nawe
kama alivyokuwa pamoja na baba yangu.
14 Lakini nitendee wema usiokoma kama
ule wa Bwana siku zote za maisha yangu,
ili nisije nikauawa, 15 [e]wala usiuondoe
wema wako kwa jamaa yangu, hata kama ni
wakati ule Bwana atakapokuwa amekatilia
mbali kila adui wa Daudi kutoka kwenye
uso wa dunia.”

16 [f]Basi Yonathani akafanya agano na
nyumba ya Daudi, akisema: “Bwana na
awaangamize adui za Daudi.” 17 [g]Naye
Yonathani akamtaka Daudi athibitishe tena
kiapo chake cha kumpenda, kwa sababu
Yonathani alimpenda Daudi kama nafsi
yake mwenyewe.

18 Kisha Yonathani akamwambia Daudi,
“Kesho ni sikukuu ya Mwezi Mwandamo.
Itajulikana kwamba haupo kwa kuwa kiti
chako kitakuwa hakina mtu. 19 [h]Kesho
kutwa, inapokaribia jioni, nenda mahali
pale ulipojificha wakati tatizo hili
lilipoanza na usubiri karibu na jiwe la
Ezeli. 20 [i]Nitapiga mishale mitatu kando
yake, kama kwamba nilikwenda kulenga
shabaha. 21 [j]Kisha nitamtuma mvulana na
kumwambia, ‘Nenda ukaitafute mishale.’
Kama nikimwambia, ‘Tazama mishale iko
upande huu wako! Uilete hapa,’ basi uje,
kwa sababu hakika kama Bwana aishivyo,
wewe ni salama, hakuna hatari. 22 Lakini
kama nikimwambia huyo mvulana,
‘Angalia, mishale iko mbele yako,’ basi
inakupasa uondoke, kwa sababu Bwana
amekuruhusu uende zako. 23 [k]Kuhusu yale
tuliyozungumza wewe na mimi: kumbuka,
Bwana ndiye shahidi kati yako wewe na
mimi milele.”

24 [l]Basi Daudi akajificha shambani, na
sikukuu ya Mwezi Mwandamo ilipowadia,
mfalme akaketi ili ale. 25 [m]Akaketi mahali
pake pa kawaida karibu na ukuta,
kuelekeana na Yonathani, naye Abneri
akaketi karibu na Mfalme Sauli, lakini kiti
cha Daudi kilikuwa wazi. 26 [n]Sauli hakusema
chochote siku ile kwa kuwa alifikiri, “Kuna
kitu cha lazima kimetokea kwa Daudi
ambacho kimemfanya najisi asihudhurie

[a]**20:7** 1Sam 10:27; 25:17; 18:11; Kum 1:23
[b]**20:8** 1Sam 18:3; 23:18; 2Sam 14:32; Yos 2:14; Rut 1:8
[c]**20:12** 1Sam 19:3; Yos 22:22
[d]**20:13** Rut 1:17; 1Sam 16:18; 18:12
[e]**20:15** 1Sam 24:21; 2Sam 9:7; Mwa 21:23
[f]**20:16** 1Sam 18:1-3; 25:22-23; Yos 22:23; 2Sam 4:7; 21:8
[g]**20:17** Yos 9:18; 1Sam 18:3; 2Sam 1:26
[h]**20:19** 1Sam 19:2
[i]**20:20** 2Fal 13:15
[j]**20:21** Kum 6:13; 10:20; Isa 65:16; Yer 4:2
[k]**20:23** Mwa 31:50
[l]**20:24** Hes 10:10; Mit 27:12
[m]**20:25** 1Sam 14:50
[n]**20:26** Law 15:5; 1Sam 16:5; Law 6:2; 7:21; Hes 19:16; 1Kor 15:33; 2Kor 6:17; Efe 2:1-3; 5:11

karamuni, hakika yeye yu najisi.” 27 Lakini siku iliyofuata, siku ya pili ya mwezi, kiti cha Daudi kilikuwa wazi tena. Kisha Sauli akamwambia mwanawe Yonathani, “Kwa nini mwana wa Yese hajaja chakulani jana wala leo?”

28 Yonathani akamjibu, “Daudi alinisihi sana nimpe ruhusa aende Bethlehemu.
29 [a]Alisema, ‘Niruhusu niende, kwa sababu jamaa yetu wana dhabihu mjini, na ndugu yangu ameniagiza niwepo huko. Kama nimepata kibali mbele yako, niruhusu niende kuona ndugu zangu.’ Hii ndiyo sababu hakuja mezani pa mfalme.”

30 Hasira ya Sauli ikawaka dhidi ya Yonathani na kumwambia, “Wewe mwana wa mwanamke mkaidi na mwasi! Je, sijui kuwa umekuwa upande wa mwana wa Yese kwa aibu yako mwenyewe na kwa aibu ya mama yako aliyekuzaa? 31 [b]Maadamu mwana wa Yese angali anaishi katika dunia hii wewe wala ufalme wako hautasimama. Sasa tuma aitwe umlete kwangu, kwa kuwa ni lazima afe!”

32 [c]Yonathani akamuuliza baba yake, “Kwa nini auawe? Kwani amefanya nini?”
33 [d]Lakini Sauli akamtupia Yonathani mkuki wake kwa nguvu ili amuue. Hapo ndipo Yonathani alipotambua kwamba baba yake alikusudia kumuua Daudi.

34 Yonathani akainuka kutoka mezani kwa hasira kali. Siku ile ya pili ya mwezi hakula chakula, kwa kuwa alikuwa amehuzunishwa na vitendo vya aibu ambavyo baba yake alikuwa anamtendea Daudi.

35 Kesho yake asubuhi Yonathani alikwenda shambani kukutana na Daudi. Alikuwa amefuatana na mvulana mdogo,
36 naye Yonathani akamwambia yule mvulana, “Kimbia ukatafute mishale nitakayorusha.” Mvulana alipokuwa akikimbia, akarusha mishale mbele yake.
37 Yule mvulana alipofika mahali pale ambapo mshale wa Yonathani ulipokuwa umeanguka, Yonathani akamwita, “Je, mshale hauko mbele yako?” 38 Yonathani akampigia kelele, “Harakisha, nenda haraka! Usisimame!” Mvulana akaokota mshale na kurudi kwa bwana wake.
39 (Mvulana hakujua chochote juu ya hayo yote; Yonathani na Daudi tu ndio waliojua.)
40 Basi Yonathani akampa yule mvulana silaha zake na kumwambia, “Nenda, zirudishe mjini.”

41 [e]Baada ya mvulana kwenda, Daudi akainuka kutoka upande wa kusini wa lile jiwe, naye akasujudu uso wake mpaka nchi mara tatu mbele ya Yonathani. Kisha kila mmoja akambusu mwenzake, wakalia pamoja. Lakini Daudi akalia zaidi.

42 [f]Yonathani akamwambia Daudi, “Nenda kwa amani, kwa kuwa tumeapiana kiapo cha urafiki kati yetu kwa jina la Bwana, tukisema, ‘Bwana ndiye shahidi kati yako na mimi, na kati ya wazao wako na wazao wangu milele.’ ” Kisha Daudi akaondoka, naye Yonathani akarudi mjini.

### *Daudi Huko Nobu*

21 [g]Daudi akaenda Nobu, kwa Ahimeleki kuhani. Ahimeleki akatetemeka alipokutana naye, akamuuliza, “Kwa nini uko peke yako? Kwa nini hukufuatana na mtu yeyote?”

2 [h]Daudi akamjibu Ahimeleki kuhani, akisema, “Mfalme ameniagiza shughuli fulani na kuniambia, ‘Mtu yeyote asijue chochote kuhusu kazi yako wala maagizo yako!’ Kuhusu watu wangu, nimewaambia tukutane mahali fulani. 3 Sasa basi, una nini mkononi? Nipatie mikate mitano au chochote unachoweza kupata.”

---

[a]**20:29** Mwa 8:20
[b]**20:31** 1Sam 23:17; 24:20
[c]**20:32** 1Sam 19:4-5; Mt 23:27; Mwa 31:36; Lk 23:22; Za 25:3; 69:4; Mit 14:25; 24:11; Mt 27:23; Yn 7:31; 15:25
[d]**20:33** 1Sam 18:11, 17
[e]**20:41** Mwa 33:3; Rut 2:10; 1Sam 24:8; 25:23; 2Sam 1:2
[f]**20:42** 1Sam 1:17; Mdo 15:33; Mwa 40:14; 2Sam 1:26; Mit 18:24; Isa 48:1; Mwa 31:50; 1Sam 18:3; 2Sam 9; 1
[g]**21:1** 1Sam 22:9; Neh 11:32; Isa 10:32; 1Sam 16:1
[h]**21:2** Mwa 27:20-24; 1Sam 19:11; 22:22; 1Fal 13:18; Za 119:29; 141:3; Mit 29:25; Gal 2:12, 13; Kol 3:9

4 [a]Lakini kuhani akamjibu Daudi, “Sina
mkate wowote wa kawaida kwa sasa. Hata
hivyo, ipo hapa mikate iliyowekwa wakfu,
iwapo watu wamejitenga na wanawake.”
5 [b]Daudi akajibu, “Hakika tumejitenga
na wanawake kwa siku hizi chache kama
kawaida ya ninapotoka kwenda kwenye
shughuli. Navyo vyombo vya wale vijana
huwa ni vitakatifu hata kwenye safari ya
kawaida, si zaidi sana leo vyombo vyao
vitakuwa ni vitakatifu?” 6 [c]Hivyo kuhani
akampa ile mikate iliyowekwa wakfu,
kwa kuwa hapakuwepo mikate mingine
isipokuwa hiyo ya Wonyesho iliyokuwa
imeondolewa hapo mbele za BWANA na
kubadilishwa na mingine yenye moto siku
ile ilipoondolewa.
7 [d]Basi siku hiyo palikuwepo na mmoja
wa watumishi wa Sauli, aliyezuiliwa mbele
za BWANA; alikuwa Doegi Mwedomu,
kiongozi wa wachunga wanyama wa Sauli.
8 Daudi akamuuliza Ahimeleki, “Je, unao
mkuki au upanga hapa? Sikuleta upanga
wala silaha nyingine yoyote, kwa sababu
shughuli ya mfalme ilikuwa ya haraka.”
9 [e]Kuhani akajibu, “Upanga wa Goliathi
Mfilisti, ambaye ulimuua katika Bonde la
Ela, upo hapa, umefungiwa katika kitambaa
nyuma ya kisibau. Kama unauhitaji,
uchukue, hakuna upanga mwingine hapa
ila huo tu.”

Daudi akasema, “Hakuna upanga
mwingine kama huo. Nipatie huo.”

*Daudi Huko Gathi*

10 [f]Siku ile Daudi akamkimbia Sauli
na kwenda kwa Akishi mfalme wa
Gathi. 11 [g]Lakini watumishi wa Akishi
wakamwambia, “Je, huyu si ndiye Daudi
mfalme wa nchi? Je, huyu si ndiye yule
ambaye wanaimba katika ngoma zao
wakisema:

“ ‘Sauli amewaua elfu zake,
naye Daudi makumi elfu yake’?”

12 Daudi akayaweka maneno haya moyoni
naye akamwogopa sana Akishi mfalme wa
Gathi. 13 [h]Basi akajifanya mwendawazimu
mbele yao; naye alipokuwa mikononi
mwao, alitenda kama kichaa, akikwaruza
kwa kutia alama juu ya milango ya lango
na kuachia udelele kutiririka kwenye ndevu
zake.
14 Akishi akawaambia watumishi wake,
“Tazameni mtu huyu! Ana wazimu! Kwa
nini mnamleta kwangu? 15 Je, mimi
nimepungukiwa na wenda wazimu kiasi
kwamba mmeniletea mtu huyo hapa
aendelee kufanya hivi mbele yangu? Je,
ilikuwa ni lazima mtu huyo aje nyumbani
kwangu?”

*Daudi Akiwa Adulamu Na Mispa*

22 [i]Daudi akaondoka Gathi na kukimbilia
kwenye pango la Adulamu. Ndugu
zake na watu wa nyumba ya baba yake
waliposikia habari hiyo, wakamwendea
huko. 2 [j]Wale wote waliokuwa katika dhiki
au waliokuwa na madeni au wale ambao
hawakuridhika wakamkusanyikia Daudi,
naye akawa kiongozi wao. Watu wapatao
400 walikuwa pamoja naye.
3 [k]Kutoka huko Daudi akaenda Mispa
huko Moabu na kumwambia mfalme wa
Moabu, “Naomba uwaruhusu baba yangu
na mama yangu waje kukaa nawe mpaka
nijue nini Mungu atakachonifanyia.”
4 [l]Hivyo akawaacha wazazi wake wakae
na mfalme wa Moabu, nao wakakaa naye
muda wote ambao Daudi alikuwa ngomeni.

[a]**21:4** Law 24:8-9; Mt 12:4; Kut 19:15; Law 15:18; 24:5; Zek 7:3
[b]**21:5** Kum 23:9-11; Yos 3:5; 2Sam 11:11; 1Tim 4:4; 1The 4:4; Law 8:26
[c]**21:6** Kut 25:30; 1Sam 22:10; Mt 12:3-4; Mk 2:25-28; Lk 6:1-5; Law 24:8
[d]**21:7** 1Sam 22:9; 14:47; Za 52
[e]**21:9** 1Sam 17:51; 17:2, 4
[f]**21:10** 1Sam 25:13; 27:2-3; 18:7
[g]**21:11** 1Sam 18:7; 29:5; Za 50
[h]**21:13** Za 34
[i]**22:1** Mwa 38:1
[j]**22:2** 1Sam 23:13; 25:13; 2Sam 15:20; Amu 11:3
[k]**22:3** Mwa 47:11; Kut 20:12; Law 19:3; Kum 5:16; Mit 10:1; 23:24; Mt 19:19; Yn 19:25-27; Efe 6:2; 1Tim 5:4
[l]**22:4** Mwa 19:37

5 [a]Ndipo nabii Gadi akamwambia Daudi,
“Usikae ngomeni. Nenda katika nchi ya
Yuda.” Hivyo Daudi akaondoka na kwenda
katika msitu wa Herethi.

*Sauli Awaua Makuhani Wa Nobu*

6 [b]Basi Sauli akasikia kwamba Daudi na
watu wake wameonekana. Sauli akiwa na
mkuki mkononi, alikuwa ameketi chini ya
mti wa mkwaju kwenye kilima huko Gibea,
maafisa wake wote wakiwa wamesimama
kumzunguka. 7 [c]Sauli akawaambia,
“Sikilizeni enyi watu wa Benyamini! Je,
mwana wa Yese atawapa ninyi nyote
mashamba na mashamba ya mizabibu?
Je, atawafanya ninyi nyote majemadari wa
maelfu na majemadari wa mamia? 8 [d]Je,
ndiyo sababu ninyi mkapanga hila mbaya
dhidi yangu? Hakuna hata mmoja wenu
ambaye ameniambia ni lini mwanangu
alifanya agano na mwana wa Yese. Hapana
hata mmoja wenu anayejishughulisha nami
wala anayeniambia kwamba mwanangu
amechochea mtumishi wangu kunivizia,
kama afanyavyo leo.”

9 [e]Lakini Doegi Mwedomu, ambaye
alikuwa akisimama na maafisa wa Sauli,
akasema, “Nilimwona mwana wa Yese akija
kwa Ahimeleki mwana wa Ahitubu huko
Nobu. 10 [f]Ahimeleki akamuuliza Bwana
kwa ajili yake; pia akampa vyakula na ule
upanga wa Goliathi Mfilisti.”

11 Kisha mfalme akatuma watu wamwite
kuhani Ahimeleki mwana wa Ahitubu,
na jamaa yote ya baba yake, waliokuwa
makuhani huko Nobu, nao wote wakaja
kwa mfalme. 12 Sauli akasema, “Sikiliza
sasa, mwana wa Ahitubu.”

Akajibu, “Naam, bwana wangu.”

13 Sauli akamwambia, “Kwa nini
umepanga shauri baya dhidi yangu, wewe
na mwana wa Yese, ukampa vyakula na
upanga, tena hukumuuliza Mungu kwa ajili
yake, na kwa sababu hiyo ameasi dhidi
yangu na kunivizia, kama afanyavyo leo?”

14 [g]Ahimeleki akamjibu mfalme, “Ni
nani miongoni mwa watumishi wako
wote aliye mwaminifu kama Daudi,
mkwewe mfalme, kiongozi wa walinzi
wako na anayeheshimika sana katika
watu wa nyumbani mwako? 15 Je, siku
hiyo ilikuwa ndiyo ya kwanza kumwomba
Mungu kwa ajili yake? La hasha! Mfalme
na usiwashutumu watumishi wako wala
yeyote wa jamaa ya baba yake, kwa kuwa
mtumishi wako hafahamu lolote kabisa
kuhusu jambo hili lote.”

16 [h]Lakini mfalme akasema, “Ahimeleki,
hakika utakufa, wewe na jamaa yote ya
baba yako.”

17 [i]Ndipo mfalme akawaamuru walinzi
wake waliokuwa kando yake: “Geukeni
na kuwaua makuhani wa Bwana, kwa
sababu nao pia wamejiunga na Daudi.
Walijua kuwa alikuwa anakimbia, wala
hawakuniambia.”

Lakini maafisa wa mfalme hawakuwa
radhi kuinua mkono kuwaua makuhani
wa Bwana.

18 [j]Kisha mfalme akamwagiza Doegi,
“Wewe geuka ukawaue makuhani.” Hivyo
basi Doegi Mwedomu, akageuka na kuwaua.
Siku ile aliwaua watu themanini na watano
wavaao visibau vya kitani. 19 [k]Pia akaupiga
Nobu kwa upanga, mji wa makuhani,
wakiwemo wanaume na wanawake, watoto
wadogo na wale wanyonyao, ng’ombe
wake, punda na kondoo.

20 [l]Lakini Abiathari, mwana wa
Ahimeleki, mwana wa Ahitubu,
akatoroka, akakimbia na kujiunga na

---

[a]**22:5** 2Sam 24:11; 1Nya 21:9; 29:29; 2Nya 29:25; 23:14
[b]**22:6** Amu 4:5; Mwa 21:23
[c]**22:7** Kum 1:15; 1Sam 8:14
[d]**22:8** 1Sam 18:3; 20:16; 23:21
[e]**22:9** 1Sam 21:7; 14:3; 21:1; Za 52
[f]**22:10** Mwa 25:22; 1Sam 23:2; 21:6; 17:51; Hes 27:21; 27:21
[g]**22:14** 1Sam 19:4; 19:5; 20:32; 24:11; Mit 31:9
[h]**22:16** 1Sam 2:31
[i]**22:17** Kut 1:17; Mdo 4:19; 5:29
[j]**22:18** 1Sam 4:17; 2:18; 2:31; Za 12:5; Mit 28:15; Kut 28:40
[k]**22:19** 1Sam 15:3; 21:1; Neh 11:32; Isa 10:32; Ay 20:19, 20; Za 10:1-18; Isa 26:13
[l]**22:20** 1Sam 23:6; 30:7; 2Sam 15:24; 20:25; 1Fal 1:7; 2:22, 26-27; 2Fal 4:4; 1Nya 15:11; 27:34; 1Sam 14:3; 2:32

Daudi. 21 Akamwambia Daudi kuwa Sauli
amewaua makuhani wa Bwana. 22 [a]Kisha
Daudi akamwambia Abiathari: “Siku ile,
wakati Doegi Mwedomu alipokuwa pale,
nilijua atahakikisha amemwambia Sauli.
Mimi ninawajibika kwa vifo vya jamaa
ya baba yako yote. 23 [b]Kaa pamoja nami;
usiogope. Mtu anayeutafuta uhai wako
anautafuta uhai wangu pia. Ukiwa pamoja
nami utakuwa salama.”

*Daudi Aokoa Keila*

23 [c]Daudi alipoambiwa kuwa, “Tazama,
Wafilisti wanapigana dhidi ya Keila
nao wanapokonya nafaka katika sakafu
za kupuria,” 2 [d]akauliza kwa Bwana,
akisema, “Je, niende na kuwashambulia
hawa Wafilisti?”

Bwana akamjibu, “Nenda, washambulie
Wafilisti na uuokoe Keila.”

3 Lakini watu wa Daudi wakamwambia,
“Hapa Yuda kwenyewe tunaogopa. Si zaidi
sana, kama tukienda Keila dhidi ya majeshi
ya Wafilisti!”

4 [e]Daudi akauliza kwa Bwana tena,
naye Bwana akamjibu akamwambia,
“Shuka uende Keila, kwa kuwa nitawatia
Wafilisti mkononi mwako.” 5 Basi Daudi na
watu wake wakaenda Keila, wakapigana
na Wafilisti na kutwaa wanyama wao wa
kutosha. Daudi akawatia hasara kubwa
Wafilisti na kuwaokoa watu wa Keila.
6 [f](Basi Abiathari mwana wa Ahimeleki
alikuwa ameleta kisibau alipokimbilia kwa
Daudi huko Keila.)

*Sauli Anamfuata Daudi*

7 [g]Sauli akaambiwa kwamba Daudi
alikuwa amekwenda Keila, naye akasema,
“Mungu amemtia mkononi mwangu, kwa
kuwa Daudi amejifunga mwenyewe kwa
kuingia kwenye mji wenye malango na
makomeo.” 8 Naye Sauli akayaita majeshi
yake yote yaende vitani, kuishukia Keila ili
kumzingira Daudi na watu wake kwa jeshi.

9 [h]Daudi alipojua kuwa Sauli alikuwa ana
hila dhidi yake, akamwambia Abiathari
kuhani, “Leta kile kisibau.” 10 [i]Daudi
akasema, “Ee Bwana, Mungu wa Israeli,
mtumishi wako amesikia kwa hakika
kwamba Sauli anapanga kuja Keila na
kuangamiza mji kwa ajili yangu. 11 Je,
watu wa Keila watanisalimisha kwake?
Je, Sauli atateremka, kama mtumishi wako
alivyosikia? Ee Bwana, Mungu wa Israeli,
mwambie mtumishi wako.”

Naye Bwana akasema, “Ndiyo,
atashuka.”

12 Daudi akauliza tena, “Je watu wa Keila
watanisalimisha mimi pamoja na watu
wangu kwa Sauli?”

Naye Bwana akasema, “Ndiyo,
watafanya hivyo.”

13 [j]Basi Daudi na watu wake, wapatao
600, wakaondoka Keila wakawa
wanakwenda sehemu moja hadi nyingine.
Sauli alipoambiwa Daudi ametoroka kutoka
Keila, hakwenda huko.

14 [k]Daudi akakaa katika ngome za
jangwani na katika vilima vya Jangwa la
Zifu. Siku baada ya siku Sauli aliendelea
kumsaka, lakini Mungu hakumtia Daudi
mikononi mwake.

15 [l]Daudi alipokuwa huko Horeshi
katika Jangwa la Zifu, akajua kuwa Sauli
alikuwa amekuja ili amuue. 16 [m]Naye
Yonathani mwana wa Sauli akamwendea
Daudi huko Horeshi na kumtia moyo
kusimama imara katika imani yake kwa

[a]**22:22** 1Sam 21:7
[b]**22:23** 1Sam 20:1
[c]**23:1** Yos 15:44; Hes 18:27; Amu 6:11
[d]**23:2** 1Sam 22; 10; 30:8; 2:1; 2Sam 5:19; Za 50:19; Hes 27:21; Amu 1:1; 1Sam 28:6; 30:8; 1Nya 10:14; 14:10; Za 32:8; 37:5; Mit 3:5, 6; Yer 10:23; Yak 1:5
[e]**23:4** 1Sam 9:16; Yos 8:7; Amu 7:7
[f]**23:6** 1Sam 22:20; 2:28; Ay 1:15-19
[g]**23:7** Kum 32:30; Za 31:21; Kut 15:9; 1Sam 24:4-6; 26:8, 9; Za 79:11
[h]**23:9** 1Sam 22:20; 2:28; 30:7
[i]**23:10** 1Sam 22:19; 2Sam 20:20; Es 3:6; Za 44:22
[j]**23:13** 1Sam 22:2; 25:13
[k]**23:14** Za 55:7; Yos 15:24; Za 54:3-4; 32:7; 11:1; Yos 15:55; 1Sam 27:1; Mit 1:16; 4:16; Kum 33:3; 1Sam 2:9; Za 32:7; 33:18; Mit 2:8; Rum 8:31; 2Tim 3:11; 4:17, 18
[l]**23:15** 1Sam 20:1
[m]**23:16** 1Sam 30:6; Za 18:2; 27:14

Mungu. 17 [a]Akamwambia, “Usiogope, Daudi;
baba yangu Sauli hatakutia mkononi
mwake. Utakuwa mfalme juu ya Israeli,
nami nitakuwa wa pili wako. Hata baba
yangu Sauli anajua hili.” 18 [b]Wote wawili
wakaweka agano mbele za BWANA. Kisha
Yonathani akaenda zake nyumbani, lakini
Daudi akabaki Horeshi.

19 [c]Basi Wazifu wakakwea kwa Sauli
huko Gibea na kusema, “Je, Daudi
hajifichi miongoni mwetu katika ngome
huko Horeshi, katika kilima cha Hakila,
kusini mwa Yeshimoni? 20 Sasa, ee mfalme,
uteremke wakati wowote unapoona vyema
kufanya hivyo, sisi tutawajibika kumkabidhi
kwa mfalme.”

21 [d]Sauli akajibu, “BWANA awabariki kwa
kunifikiria. 22 Nendeni mkafanye maandalizi
zaidi. Mkajue mahali ambapo Daudi huenda
mara kwa mara na nani amepata kumwona
huko. Wananiambia yeye ni mwerevu sana.
23 [e]Jueni kila mahali anapojificha mrudi na
kunipa taarifa kamili. Kisha nitakwenda
pamoja nanyi; kama atakuwa katika eneo
hilo, nitamsaka miongoni mwa koo zote
za Yuda.”

24 [f]Basi wakaondoka na kwenda mpaka
Zifu wakimtangulia Sauli. Naye Daudi na
watu wake walikuwa katika Jangwa la
Maoni, katika Araba kusini mwa Yeshimoni.
25 Sauli na watu wake wakaanza msako,
naye Daudi alipoelezwa hili, akateremka
mpaka mwambani na kukaa katika Jangwa
la Maoni. Sauli aliposikia hili, akaenda
katika Jangwa la Maoni akimfuata Daudi.

26 [g]Sauli alikuwa akienda upande mmoja
wa mlima, naye Daudi na watu wake
walikuwa upande mwingine wa mlima,
wakiharakisha kumkimbia Sauli. Wakati
Sauli na majeshi yake walipokaribia
kumkamata Daudi na watu wake,
27 [h]mjumbe alikuja kwa Sauli, akisema,
“Njoo haraka! Wafilisti wanaishambulia
nchi.” 28 Ndipo Sauli akarudi akaacha
kumfuata Daudi na kwenda kukabiliana na
Wafilisti. Ndiyo sababu wanaiita sehemu hii
Sela-Hamalekothi.[i] 29 [j]Naye Daudi akakwea
kutoka huko na kuishi katika ngome za
En-Gedi.

### *Daudi Amwacha Sauli Hai*

24 [k]Baada ya Sauli kurudi kuwafuatia
Wafilisti, akaambiwa kwamba, “Daudi
yuko katika Jangwa la En-Gedi.” 2 [l]Basi
Sauli akachukua watu hodari 3,000 kutoka
Israeli yote kwenda kumsaka Daudi na watu
wake karibu na Majabali ya Mbuzi-Mwitu.

3 [m]Akaja mpaka kwenye mazizi ya kondoo
kando ya njia, hapo palikuwa na pango,
na Sauli akaingia ndani kujipumzisha.
Daudi na watu wake walikuwa wamo
mle pangoni kwa ndani zaidi. 4 [n]Watu wa
Daudi wakasema, “Hii ndiyo siku aliyonena
BWANA akikuambia, ‘Nitamtia adui yako
mikononi mwako ili wewe umtendee
utakavyo.’ ” Basi Daudi akanyemelea bila
kuonekana na kukata upindo wa joho la
Sauli.

5 [o]Baada ya hilo, dhamiri ya Daudi
ikataabika kwa kukata upindo wa joho la
Sauli. 6 [p]Akawaambia watu wake, “BWANA
na apishie mbali nisije nikafanya jambo
kama hilo kwa bwana wangu, yeye ambaye
ni mpakwa mafuta wa BWANA, au kuinua
mkono wangu dhidi yake; kwani yeye
ni mpakwa mafuta wa BWANA.” 7 [q]Kwa

---

[a]**23:17** 1Sam 20:31; 24:20
[b]**23:18** 1Sam 18:3; 2Sam 9:1; 21:7
[c]**23:19** 1Sam 26:1; Za 54; 1Sam 26:3
[d]**23:21** Rut 2:20; 2Sam 2:5; 1Sam 22:8
[e]**23:23** Mwa 31:36
[f]**23:24** Yos 15:55; 1Sam 26:1; 25:2
[g]**23:26** Za 17:6; 1Sam 19:12; 20:38; 2Sam 15:14; Za 31:22; 2Nya 20:12; 2Kor 1:8
[h]**23:27** Kum 32:36; 1Sam 14:6; 2Sam 22:1-51; 2Fal 19:9; Za 18:1-50; Isa 37:6-9; 59:1; Yer 15:20, 21
[i]28 Sela-Hamalekothi maana yake Mwamba wa Kutengana.
[j]**23:29** 1Sam 24:22; Yos 15:62; 2Nya 20:2; Wim 1:14
[k]**24:1** Yos 15:62; 1Sam 23:28-29
[l]**24:2** 1Sam 26:2; Za 38:12
[m]**24:3** Amu 3:24
[n]**24:4** 1Sam 25:28-30; 2Sam 4:8; 1Sam 23; 17; 26:8
[o]**24:5** 1Sam 26:9; 2Sam 24:10
[p]**24:6** Mwa 26:11; 1Sam 12:3; 26:11; 2Sam 1:14; Ay 31:29, 30
[q]**24:7** Za 7:4; Mt 5:44; Rum 12:17

maneno haya Daudi akawaonya watu
wake na hakuwaruhusu wamshambulie
Sauli. Naye Sauli akaondoka pangoni na
kwenda zake.
8 [a]Ndipo Daudi naye akatoka pangoni na
kumwita Sauli akisema, “Mfalme, bwana
wangu!” Sauli alipotazama nyuma, Daudi
akainama na kusujudu uso wake mpaka
nchi. 9 [b]Akamwambia Sauli, “Kwa nini
unasikiliza wakati watu wanapokuambia,
‘Daudi amenuia kukudhuru’? 10 Leo umeona
kwa macho yako mwenyewe jinsi Bwana
alivyokutia mikononi mwangu huko
pangoni. Watu wengine walisisitiza nikuue,
lakini nilikuacha, nikisema, ‘Sitainua
mkono wangu dhidi ya bwana wangu, kwa
sababu yeye ni mpakwa mafuta wa Bwana.’
11 [c]Tazama, baba yangu, ona kipande hiki
cha joho lako mkononi mwangu! Nilikata
upindo wa joho lako lakini sikukuua.
Basi ujue na kutambua kuwa sina hatia
ya kutenda mabaya wala ya kuasi. Wewe
sijakukosea, lakini wewe unaniwinda
mimi ili kuuondoa uhai wangu. 12 [d]Bwana
na ahukumu kati yangu na wewe. Naye
Bwana alipize mabaya unayonitendea,
lakini mkono wangu hautakugusa. 13 [e]Kama
msemo wa kale usemavyo, ‘Kutoka kwa
watenda maovu hutoka matendo maovu,’
kwa hiyo mkono wangu hautakugusa wewe.
14 [f]“Je, mfalme wa Israeli ametoka dhidi
ya nani? Ni nani unayemfuatia? Je, ni
mbwa mfu? Ni kiroboto? 15 [g]Bwana na awe
mwamuzi wetu, yeye na aamue kati yetu.
Yeye na anitetee shauri langu; anihesabie
haki kwa kuniokoa mkononi mwako.”
16 [h]Daudi alipomaliza kusema haya, Sauli
akamuuliza, “Je, hiyo ni sauti yako, Daudi
mwanangu?” Ndipo Sauli akalia kwa sauti
kuu, akisema, 17 [i]“Wewe ni mwenye haki
kuliko mimi; umenitendea mema, lakini
mimi nimekutendea mabaya. 18 [j]Sasa
umeniambia juu ya mema uliyonitendea.
Bwana alinitia mikononi mwako, lakini
wewe hukuniua. 19 [k]Je, mtu ampatapo
adui yake, humwacha aende zake bila
kumdhuru? Bwana na akulipe mema kwa
jinsi ulivyonitenda leo. 20 [l]Ninajua kwamba
hakika utakuwa mfalme na ya kwamba
ufalme wa Israeli utakuwa imara mikononi
mwako. 21 [m]Sasa niapie kwa Bwana kwamba
hutakatilia mbali uzao wangu wala kulifuta
jina langu kutoka jamaa ya baba yangu.”
22 [n]Basi Daudi akamwapia Sauli. Kisha
Sauli akarudi zake nyumbani, lakini Daudi
na watu wake wakapanda kwenda ngomeni.

*Daudi, Nabali Na Abigaili*

25 [o]Basi Samweli akafa, nao Israeli wote
wakakusanyika na kumwombolezea;
wakamzika nyumbani kwake huko Rama.
Kisha Daudi akateremka kwenye Jangwa
la Maoni. 2 [p]Mtu mmoja huko Maoni,
aliyekuwa na makao huko Karmeli, alikuwa
tajiri sana. Alikuwa na mbuzi elfu moja
na kondoo elfu tatu, aliokuwa akiwakata
manyoya huko Karmeli. 3 [q]Jina la mtu
huyo lilikuwa Nabali, naye mkewe aliitwa
Abigaili. Alikuwa mwanamke mwenye
busara na mzuri wa sura, lakini mumewe,
ambaye alikuwa wa ukoo wa Kalebu,
alikuwa mwenye hasira na mchoyo katika
utendaji wake.
4 [r]Daudi alipokuwa huko jangwani,

[a]**24:8** 1Sam 20:41; 25:23-24
[b]**24:9** Za 141:6; Mit 16:28; 17:9
[c]**24:11** Za 7:3; 1Sam 25:28; Za 35:7; Mwa 31:36; 1Sam 26:20; 20:1
[d]**24:12** Mwa 16:5; 1Sam 25:38; Ay 9:15; Hes 31:3; Amu 11:27
[e]**24:13** Mt 7:20
[f]**24:14** 1Sam 17:43; 26:20; 2Sam 9:8; Ay 32:9; Mit 5:23
[g]**24:15** Za 35:1, 23; Isa 49:25; Za 26:1; 35:24; 43:1; 50:4; 54:1; 135:14; 119:134; 2Sam 9:8
[h]**24:16** 1Sam 16:17; 26:17
[i]**24:17** Mwa 38:26; Mt 5:44; Kut 9:27; 1Sam 26:21
[j]**24:18** 1Sam 26:23
[k]**24:19** Rut 2:12; 2Nya 15:7
[l]**24:20** 1Sam 20:31; 13:14; 23:17; 23:17; 2Sam 3:17; Ay 15:25; Mt 2:3-6, 13, 14
[m]**24:21** Mwa 21:23; 47:31; 1Sam 18:3; 2Sam 21:1-9; 1Sam 20:14-15
[n]**24:22** 1Sam 23:29
[o]**25:1** 1Sam 28:3; Law 10:6; Hes 20:29; Kum 34:8; Mwa 21:2; 1Sam 7:17; 2Nya 33:20
[p]**25:2** Yos 15:55; 2Sam 19:32; Mwa 31:19; 1Sam 23:24; Mwa 38:13; 2Sam 13:23
[q]**25:3** Mit 31:10; Yos 14:13; 15:13; Rut 4:11; Mit 14:1; 24:3, 4; Isa 32:5, 7
[r]**25:4** Mwa 38:13; 2Sam 13:23

akasikia kuwa Nabali alikuwa anakata
kondoo manyoya. 5 [a]Basi akatuma vijana
kumi na kuwaambia, "Pandeni kwa Nabali
huko Karmeli, mkamsalimie kwa jina
langu. 6 [b]Mwambieni: 'Amani iwe kwako!
Amani iwe kwako pamoja na wa nyumbani
mwako! Pia amani iwe pamoja na vyote
ulivyo navyo!

7 " 'Nasikia kuwa huu ni wakati wa kukata
kondoo manyoya. Wachunga mifugo wako
walipokuwa pamoja nasi, hatukuwatendea
mabaya na wakati wote waliokuwa
huko Karmeli hakuna chochote chao
kilipotea. 8 [c]Waulize watumishi wako nao
watakuambia. Kwa hiyo uwatendee wema
vijana wangu, kwani tumekuja wakati wa
furaha. Tafadhali wape watumishi wako
na mwanao Daudi chochote kitakachokuja
mkononi mwako kwa ajili yao.' "

9 Watu wa Daudi walipofika wakampa
Nabali ujumbe huu kwa jina la Daudi. Kisha
wakangojea.

10 [d]Nabali akawajibu watumishi wa Daudi,
"Huyu Daudi ni nani? Huyu mwana wa Yese
ni nani? Watumishi wengi wanakimbia
kutoka kwa bwana zao siku hizi. 11 [e]Kwa
nini nichukue mkate wangu, maji yangu
na nyama niliyochinja kwa ajili ya wakata
manyoya wangu, na kuwapa watu ambao
hakuna anayejua wanakotoka?"

12 Watu wa Daudi wakageuka na kurudi.
Walipofika, wakaarifu kila neno. 13 [f]Daudi
akawaambia watu wake, "Jifungeni panga
zenu!" Basi wakajifunga panga zao, naye
Daudi akajifunga upanga wake. Watu kama
mia nne hivi wakapanda pamoja na Daudi,
na watu mia mbili wakabaki na vifaa.

14 [g]Mmoja wa watumishi akamwambia
Abigaili, mkewe Nabali: "Daudi
alituma wajumbe kutoka jangwani
kumpa bwana wetu salamu zake, lakini
akawavurumishia matukano. 15 Hata hivyo
watu hawa walikuwa wema sana kwetu.
Hawakututendea mabaya, na wakati wote
tulipokuwa nje huko mashambani karibu
nao, hatukupotewa na kitu chochote.
16 [h]Usiku na mchana walikuwa ukuta
wakituzunguka wakati wote tulipokuwa
tukichunga kondoo zetu karibu nao. 17 [i]Sasa
fikiri juu ya jambo hili na uone unaweza
kufanya nini, kwa sababu maafa yanakaribia
juu ya bwana wetu na nyumba yake yote.
Yeye ni mtu mwovu kiasi kwamba hakuna
mtu awezaye kuzungumza naye."

18 [j]Abigaili akafanya haraka, akachukua
mikate mia mbili, viriba viwili vya divai,
kondoo watano waliochinjwa vipimo vitano
vya bisi, vishada mia moja vya zabibu kavu,
mikate mia mbili ya tini, akavipakia juu
ya punda. 19 [k]Kisha akawaambia watumishi
wake, "Tangulieni; mimi nitakuja nyuma
yenu." Lakini hakumwambia Nabali
mumewe.

20 Ikawa alipokuwa amepanda punda
wake kwenye bonde la mlima, tazama,
Daudi na watu wake wakawa wanateremka
kumwelekea, naye akakutana nao.
21 [l]Daudi alikuwa amesema, "Ilikuwa ni
kazi bure kuchunga kwangu kote mali za
huyu mtu huko jangwani hivi kwamba
hakuna chochote chake kilichopotea.
Yeye amenilipa baya kwa ajili ya wema.
22 [m]BWANA na amshughulikie Daudi,
tena kwa ukali, ikiwa kesho asubuhi
nitambakizia mwanaume hata mmoja aliye
hai miongoni mwa watu wake wote!"

23 [n]Abigaili alipomwona Daudi, akashuka
haraka kwenye punda wake, akainama
kifudifudi uso wake mpaka nchi mbele ya
Daudi. 24 [o]Akamwangukia miguuni pake na
kusema: "Bwana wangu, kosa hili na liwe

[a]**25:5** 1Sam 18:28; Lk 10:5
[b]**25:6** Za 122:7; Mt 10:12; 1Nya 12:18
[c]**25:8** Neh 8:10; Es 9:19
[d]**25:10** Amu 9:28; Za 73:7, 8; 123:3, 4
[e]**25:11** Amu 8:6
[f]**25:13** 1Sam 22:2; 21:10; 23:13; 30:24; Hes 31:27
[g]**25:14** 1Sam 13:10
[h]**25:16** Kut 14:22; Ay 1:10; Za 139:5; Zek 2:5
[i]**25:17** Kum 13:13; 1Sam 20:7
[j]**25:18** Law 23:14; 1Sam 17:17; 1Nya 12:40; Mwa 42:26; 2Sam 16:1; Isa 30:6
[k]**25:19** Mwa 32:20; 1Sam 25:36
[l]**25:21** Za 109:5; 1Sam 19:4; Mwa 44:4; Za 35:12; Mit 17:13; Yer 18:20; 1Pet 2:20; 3:17
[m]**25:22** Rut 1:17; 1Fal 14:10; 21:21; 2Fal 9:8; 1Sam 20:13
[n]**25:23** Mwa 19:1; 1Sam 20:41; Yos 15:18; Amu 1:14
[o]**25:24** 2Sam 14:9

juu yangu mwenyewe. Tafadhali mruhusu
mtumishi wako aseme nawe. Sikia kile
mtumishi wako atakachosema. 25 [a]Bwana
wangu na asimjali huyo mtu mwovu Nabali.
Yeye anafanana na jina lake; jina lake ni
Mpumbavu, nao upumbavu huenda pamoja
naye. Lakini kwangu mimi, mtumishi wako,
sikuwaona hao watu waliotumwa na bwana
wangu.

26 [b]"Basi sasa, kwa kuwa BWANA
amekuzuia, wewe bwana wangu,
kutokumwaga damu na kutolipiza kisasi
kwa mikono yako mwenyewe, hakika kama
BWANA aishivyo na kama uishivyo, maadui
zako na wote wanaokusudia kumdhuru
bwana wangu wawe kama Nabali. 27 [c]Nayo
zawadi hii ambayo mtumishi wako
amemletea bwana wangu, wapewe watu
wanaofuatana nawe. 28 [d]Tafadhali samehe
kosa la mtumishi wako, kwa kuwa BWANA
kwa hakika ataifanya imara nyumba ya
ufalme kwa bwana wangu, kwa sababu
anapigana vita vya BWANA. 29 [e]Hata ingawa
yuko mtu anayekufuatia kuuondoa uhai
wako, usiruhusu baya lolote kuonekana
kwako siku zote za maisha yako, uhai wa
bwana wangu utafungwa salama kwenye
furushi la walio hai na BWANA Mungu wako.
Lakini uhai wa adui zako atavurumishwa
kama vile jiwe kutoka kwenye kombeo.
30 [f]BWANA atakapokuwa ameshamtendea
bwana wangu kila kitu chema alichoahidi
kumhusu yeye na kumweka kuwa kiongozi
wa Israeli, 31 [g]bwana wangu hatakuwa
na dhamiri inayolemewa na mzigo kwa
kumwaga damu kusiko na sababu, au
kujilipizia kisasi yeye mwenyewe. BWANA
atakapomletea bwana wangu mafanikio,
umkumbuke mtumishi wako."

32 [h]Daudi akamwambia Abigaili,
"Ahimidiwe BWANA, Mungu wa Israeli
aliyekutuma kunilaki leo. 33 Ubarikiwe
kwa uamuzi wako mzuri na kwa kunizuia
nisimwage damu leo na kulipiza kisasi
kwa mikono yangu. 34 La sivyo, hakika
kama BWANA, Mungu wa Israeli, aishivyo,
ambaye amenizuia nisiwadhuru, kama
usingekuja haraka kunilaki, hakuna hata
mwanaume mmoja wa Nabali angeachwa
hai kufikia mapambazuko."

35 [i]Ndipo Daudi akapokea kutoka mkononi
mwake kile alichokuwa amemletea, naye
akasema, "Nenda nyumbani kwako kwa
amani; nimesikia maneno yako na kukujalia
ombi lako."

36 [j]Abigaili alipokwenda kwa Nabali,
alikuwa ndani ya nyumba yake akifanya
karamu kama ile ya mfalme. Naye alikuwa
ana furaha nyingi, akiwa amelewa sana.
Kwa hiyo Abigaili hakumwambia mumewe
kitu chochote mpaka asubuhi yake. 37 [k]Basi
asubuhi, Nabali alipokuwa amelevuka,
mkewe akamwambia mambo yote, nao
moyo wake ukazimia, akawa kama jiwe.
38 [l]Baada ya siku kumi, BWANA akampiga
Nabali, naye akafa.

39 [m]Daudi aliposikia kwamba Nabali
amekufa, akasema, "Ahimidiwe BWANA,
ambaye amenitetea shauri langu dhidi ya
Nabali kwa kuwa alinitendea kwa dharau.
Amemzuia mtumishi wake asitende mabaya
na BWANA ameuleta ubaya wa Nabali juu
ya kichwa chake mwenyewe."

Kisha Daudi akatuma ujumbe kwa
Abigaili kumwomba awe mke wake.
40 Watumishi wa Daudi wakaenda mpaka
Karmeli na kumwambia Abigaili, wakisema,

---

[a]**25:25** Mit 17:12; 12:16; 14:16; 20:3; Isa 32:5
[b]**25:26** Ebr 10:30; 2Sam 18:32; 2Fal 2:2; Mwa 20:6; Rum 12:19; 2Sam 18:32
[c]**25:27** Mwa 33:11; 1Sam 30:26
[d]**25:28** 2Sam 14:9; 7:11, 26; 1Sam 18:17; 24:11; 1Fal 9:5; 1Nya 17:16
[e]**25:29** 1Sam 20:1; Yer 10:18; 22:26; 1Sam 17:50; 2Sam 4:8; Za 66:9; Mit 10:29, 30; Mdo 17:28
[f]**25:30** 1Sam 12:12; 13:14
[g]**25:31** Mwa 40:14; 2Sam 3:10
[h]**25:32** Mwa 24:27; Kut 18:10; Lk 1:68; Ezr 7:27; Za 41:12, 13; 72:18; 2Kor 8:16
[i]**25:35** Mwa 19:21; 2Fal 5:19; 1Sam 20:42; 2Sam 15:9; Lk 7:50
[j]**25:36** Rut 3:7; Mit 20:1; Mhu 10:17; Isa 5:11, 22; 22:13; 28:7; 56:12; Hos 4; 11; 2Sam 13:23
[k]**25:37** Kut 15:16; Kum 28:28; Ay 15:21
[l]**25:38** Kum 32:35; 1Sam 24:12; 26:10; 2Sam 6:7; 12:15; Kut 12:29; 2Sam 6:7; Ay 12:10; Za 104:29; Mdo 12:23
[m]**25:39** Mit 22:23; 2Sam 3:28, 29; 1Fal 2:44; Es 7:10; Za 7:16

"Daudi ametutuma kwako kukuchukua uwe
mkewe."
41 [a]Akainama chini uso wake mpaka
ardhini, akasema, "Mjakazi wako yuko
hapa, tayari kuwatumikia na kuwanawisha
miguu watumishi wa bwana wangu."
42 [b]Abigaili akainuka kwa haraka, akapanda
punda wake, akihudumiwa na wajakazi
wake watano, akaenda pamoja na wajumbe
wa Daudi, naye akawa mkewe. 43 [c]Pia Daudi
alikuwa amemwoa Ahinoamu wa Yezreeli,
wote wawili wakawa wake zake. 44 [d]Lakini
Sauli alikuwa amemwoza Mikali binti yake,
aliyekuwa mkewe Daudi, kwa Palti mwana
wa Laishi, kutoka Galimu.

### *Daudi Amwacha Sauli Hai Tena*

26 [e]Hao Wazifu wakamwendea Sauli
huko Gibea na kusema, "Je, Daudi
hakujificha katika kilima cha Hakila,
kinachotazamana na Yeshimoni?"
2 [f]Hivyo Sauli akashuka kwenda katika
Jangwa la Zifu, akiwa na watu wake 3,000
wa Israeli waliochaguliwa, kumsaka Daudi
huko. 3 [g]Sauli akapiga kambi yake kando
ya barabara juu ya kilima cha Hakila
kinachotazamana na Yeshimoni, lakini
Daudi alikuwa anaishi huko jangwani.
Alipoona kuwa Sauli amemfuata huko,
4 Daudi akatuma wapelelezi na akapata
habari kwa hakika kwamba Sauli alikuwa
amewasili.
5 [h]Ndipo Daudi akaondoka, akaenda
hadi mahali Sauli alikuwa amepiga kambi.
Akaona mahali Sauli na Abneri mwana
wa Neri, jemadari wa jeshi, walipokuwa
wamelala. Sauli alikuwa amelala ndani ya
kambi, jeshi likiwa limemzunguka.
6 [i]Basi Daudi akamuuliza Ahimeleki Mhiti,
na Abishai mwana wa Seruya, nduguye
Yoabu, akisema, "Ni nani atakayeshuka
pamoja nami kambini kwa Sauli?"
Abishai akajibu, "Nitakwenda pamoja
nawe."
7 Hivyo Daudi na Abishai wakaenda
kwenye jeshi wakati wa usiku, tazama
Sauli, alikuwa amelala ndani ya kambi na
mkuki wake umekitwa ardhini karibu na
kichwa chake. Abneri na askari walikuwa
wamelala kumzunguka Sauli.
8 [j]Abishai akamwambia Daudi, "Leo
Mungu amemtia adui yako mikononi
mwako. Sasa niruhusu nimchome mpaka
ardhini kwa pigo moja la mkuki wangu;
sitamchoma mara mbili."
9 [k]Lakini Daudi akamwambia Abishai,
"Usimwangamize! Ni nani awezaye kutia
mkono juu ya mpakwa mafuta wa Bwana
na asiwe na hatia?" 10 [l]Daudi akasema,
"Hakika kama vile Bwana aishivyo,
Bwana mwenyewe atampiga; au wakati
wake utafika, naye atakufa, au atakwenda
vitani na kuangamia. 11 [m]Lakini Mungu na
apishie mbali nisije nikainua mkono juu ya
mpakwa mafuta wa Bwana. Sasa chukua
huo mkuki na hilo gudulia la maji vilivyo
karibu na kichwa chake, tuondoke."
12 [n]Hivyo Daudi akachukua huo mkuki na
hilo gudulia la maji vilivyokuwa karibu na
kichwa cha Sauli, nao wakaondoka. Hakuna
yeyote aliyeona au kufahamu habari hii,
wala hakuna hata mmoja aliyeamka
usingizini. Wote walikuwa wamelala, kwa
sababu Bwana alikuwa amewatia kwenye
usingizi mzito.
13 Kisha Daudi akavuka upande mwingine

[a]**25:41** Rut 2:10, 13; Mit 15:33; 18:12
[b]**25:42** 2Sam 2:2; 3:3; 1Nya 3:1
[c]**25:43** 2Sam 3:2; 1Nya 3:1; 1Sam 30:5; 2Sam 2:2; Yos 15:56
[d]**25:44** 2Sam 3:15; Isa 10:30
[e]**26:1** 1Sam 23:19; Za 54; 1Sam 23:24
[f]**26:2** 1Sam 24:2; 13:2
[g]**26:3** 1Sam 12:19
[h]**26:5** 1Sam 17:55; 14:50
[i]**26:6** Mwa 10:15; 2Sam 2:18; 10:10; 16:9; 18:2; 19:21; 23:18; 1Nya 11:20; 19:11; 2:16; Amu 7:10-11
[j]**26:8** 1Sam 24:18
[k]**26:9** Mwa 26:11; 1Sam 9:16; 2Sam 1:14; 19:21; Mao 4:20; 1Sam 24:5
[l]**26:10** Mwa 16:5; 1Sam 25:38; Rum 12:19; Za 37:13; 31:6; 2Sam 1:1; Za 94:1, 2, 23; Mit 20:22; Lk 18:7; Rum 12:19; Ebr 10:30; Ufu 18:8; Kum 31:14; Ay 7:1; 14:5
[m]**26:11** Law 19:8; 1Sam 24:6, 12; Mit 24:29; Rum 12:17, 19; Yak 5:5-11; 1Pet 3:9
[n]**26:12** Amu 4:21; Mwa 2:21; Es 6:1; Isa 29:10

na kusimama juu ya kilima mahali palipokuwa na nafasi pana kati yao. 14 Daudi akalipigia kelele jeshi na Abneri mwana wa Neri, akisema, “Je, Abneri, hutanijibu?”

Abneri akajibu, “Nani wewe umwitaye mfalme?”

15 Daudi akasema, “Wewe si ni mtu shujaa? Ni nani aliye kama wewe katika Israeli? Kwa nini basi hukumlinda mfalme bwana wako? Mtu mmoja alikuja kumwangamiza mfalme, bwana wako. 16 Ulichokifanya si kizuri. Kwa hakika kama aishivyo Bwana, wewe na watu wako mnastahili kufa, kwa sababu hamkumlinda bwana wenu, mpakwa mafuta wa Bwana. Tazameni hapo mlipo. Uko wapi mkuki wa mfalme na gudulia la maji ambavyo vilikuwa karibu na kichwa chake?”

17 [a]Sauli akatambua sauti ya Daudi, na kusema, “Je, hiyo ni sauti yako, Daudi mwanangu?”

Daudi akajibu, “Naam, hiyo ndiyo, bwana wangu mfalme.” 18 [b]Pia akaongeza, “Kwa nini bwana wangu anamfuatia mtumishi wake? Nimefanya nini, nalo kosa langu ni lipi nililolifanya niwe na hatia? 19 [c]Sasa mfalme bwana wangu na asikilize maneno ya mtumishi wake. Kama Bwana amekuchochea dhidi yangu, basi yeye na aipokee sadaka yangu. Lakini hata hivyo, kama ni wanadamu waliofanya hivyo, walaaniwe mbele za Bwana! Wao sasa wamenifukuza kutoka sehemu yangu katika urithi wa Bwana wangu wakisema, ‘Nenda ukatumikie miungu mingine.’ 20 [d]Basi usiache damu yangu imwagike kwenye ardhi mbali na uso wa Bwana. Mfalme wa Israeli ametoka kutafuta kiroboto, kama vile mtu awindavyo kware katika milima.”

21 [e]Ndipo Sauli akasema, “Nimetenda dhambi. Rudi, Daudi mwanangu. Kwa kuwa uliyahesabu maisha yangu kuwa ya thamani leo, sitajaribu kukudhuru tena. Hakika nimetenda kama mpumbavu na nimekosa sana.”

22 Daudi akajibu, “Mkuki wa mfalme uko hapa. Mmoja wa vijana wako na avuke kuuchukua. 23 [f]Bwana humlipa kila mtu kwa ajili ya haki yake na uaminifu wake. Bwana alikutia katika mikono yangu leo, lakini sikuinua mkono wangu juu ya mpakwa mafuta wa Bwana. 24 [g]Kwa hakika kama vile maisha yako yalivyokuwa ya thamani kwangu leo, vivyo hivyo maisha yangu na yawe na thamani kwa Bwana na kuniokoa kutoka taabu zote.”

25 [h]Ndipo Sauli akamwambia Daudi, “Mwanangu Daudi na ubarikiwe; utafanya mambo makubwa na hakika utashinda.”

Basi Daudi akaenda zake, naye Sauli akarudi nyumbani.

### *Daudi Miongoni Mwa Wafilisti*

27 Daudi akasema moyoni mwake, “Katika mojawapo ya siku hizi nitaangamizwa kwa mkono wa Sauli. Jambo lililo bora ni kutorokea kwenye nchi ya Wafilisti. Hivyo Sauli atakata tamaa ya kunisaka popote katika Israeli, nami nitakuwa nimeponyoka mkononi mwake.”

2 [i]Hivyo Daudi akaondoka na hao watu mia sita waliokuwa pamoja naye na kwenda kwa Akishi mwana wa Maoki mfalme wa Gathi. 3 [j]Daudi na watu wake wakakaa huko Gathi pamoja na Akishi. Kila mtu alikuwa pamoja na jamaa yake, naye Daudi pamoja na wakeze wawili: yaani Ahinoamu wa Yezreeli, na Abigaili wa Karmeli, mjane wa Nabali. 4 Sauli alipokuwa ameambiwa

[a]**26:17** 1Sam 24:16
[b]**26:18** Ay 13:23; Yer 37:18; 1Sam 24:9, 11; Za 7:3
[c]**26:19** 1Sam 24:9; 2Sam 16:11; Kum 20:16; 2Sam 14:16; 20:19; 21:3; Kum 4:28; 11:28; Za 120:5; Kut 15:17; Kum 4:20; 9:26; Za 106:4, 5; Isa 19:25
[d]**26:20** 1Sam 24:11; 24:14; Yer 4:29; 16:16; Amo 9:3
[e]**26:21** Kut 9:27; Za 72:14; 1Sam 15:24; 24:17; Hes 22:34; 1Sam 15:24; 24:17; Mt 27:4
[f]**26:23** Mwa 16:5; Rut 2:21; Za 62:12; 2Sam 22:21-25; Za 18:20-24; 1Sam 24:18; Mhu 8:12; Isa 3:10-11
[g]**26:24** Za 54:7
[h]**26:25** Rut 2:12
[i]**27:2** 1Sam 30:9; 2:3; 21:10; 1Fal 2:39; 1Sam 25:13
[j]**27:3** 1Sam 25:43; 30:3

kwamba Daudi alikuwa amekimbilia Gathi,
hakuendelea kumsaka tena.
5 Ndipo Daudi akamwambia Akishi,
“Kama nimepata kibali machoni pako,
unipe sehemu katika mojawapo ya miji
katika nchi nikae huko. Kwa nini mtumwa
wako akae pamoja nawe katika mji huu
wa kifalme?”
6 [a]Hivyo siku hiyo Akishi akampa Daudi
mji wa Siklagi, nao Siklagi umekuwa mali
ya wafalme wa Yuda tangu wakati huo.
7 [b]Daudi akaishi katika nchi ya Wafilisti
muda wa mwaka mmoja na miezi minne.
8 [c]Basi Daudi na watu wake wakapanda
na kuwashambulia Wageshuri, Wagirizi na
Waamaleki. (Tangu zamani haya mataifa
yalikuwa yameishi kwenye eneo lililotanda
kuanzia Telemu katika njia iteremkayo Shuri
hadi kufikia nchi ya Misri.) 9 [d]Kila mara
Daudi aliposhambulia eneo, hakubakiza
hai mwanaume wala mwanamke, lakini
alichukua kondoo na ng’ombe, punda na
ngamia, na nguo. Kisha akarudi kwa Akishi.
10 [e]Akishi alipomuuliza, “Je leo
umeshambulia wapi?” Daudi humjibu,
“Dhidi ya Negebu ya Yuda,” au wakati
mwingine husema, “Dhidi ya Negebu
ya Yerameeli,” au “Dhidi ya Negebu
ya Wakeni.” 11 Daudi hakumwacha hai
mwanaume au mwanamke ili apate
kuletwa Gathi, kwa maana Daudi aliwaza,
“Wanaweza kujulisha habari zetu na
kusema, ‘Hivi ndivyo alivyofanya Daudi.’ ”
Hii ndiyo ilikuwa desturi yake wakati wote
aliishi katika nchi ya Wafilisti. 12 [f]Akishi
akamsadiki Daudi na kuwaza moyoni
mwake, akasema, “Daudi amekuwa kitu
cha kuchukiza kabisa kwa watu wake,
Waisraeli, hivi kwamba atakuwa mtumishi
wangu milele.”

[a]**27:6** Yos 15:31; 19:5; 1Sam 30:1; 1Nya 12:30; Neh 11:28
[b]**27:7** 1Sam 29:3
[c]**27:8** Yos 12:5; Kut 17:14, 16; 1Sam 14:48; 30:1; 2Sam 1:8; 8:12; Mwa 16:5; Kut 15:22; Yos 13:2; Amu 1:29; Mwa 25:18
[d]**27:9** 1Sam 15:3
[e]**27:10** 1Sam 30:29; Amu 1:16; 1Nya 2:9, 25; Za 14:3; Mit 29:25
[f]**27:12** Mwa 34:30; 1Sam 29:6

### *Sauli Na Mchawi Wa Endori*

28 [g]Siku zile Wafilisti wakakusanya
majeshi yao ili kupigana vita dhidi ya
Israeli. Akishi akamwambia Daudi, “Lazima
ujue kuwa wewe pamoja na watu wako
mtafuatana nami kwenda vitani.”
2 [h]Daudi akasema, “Ndipo wewe
mwenyewe utakapojionea jambo ambalo
mtumishi wako anaweza kufanya.”
Akishi akamjibu Daudi, “Vyema sana,
mimi nitakufanya uwe mlinzi wangu
daima.”
3 [i]Wakati huo Samweli alikuwa
amekufa, nao Israeli wote walikuwa
wamemwombolezea na kumzika kwenye
mji wake mwenyewe huko Rama. Sauli
alikuwa amewafukuza waaguzi na wachawi.
4 [j]Wafilisti wakakusanyika na kupiga
kambi yao huko Shunemu, naye Sauli
akawakusanya Waisraeli wote na kupiga
kambi yao huko Gilboa. 5 [k]Sauli alipoona
jeshi la Wafilisti, akaogopa; moyo wake
ukajawa na hofu kuu. 6 [l]Ndipo Sauli
akauliza ushauri kwa BWANA, lakini BWANA
hakumjibu kwa ndoto, wala kwa Urimu,[m]
wala kwa njia ya manabii. 7 [n]Basi Sauli
akawaambia watumishi wake, “Nitafutieni
mwanamke mwaguzi ili nimwendee, nipate
kuuliza kwake.”
Watumishi wake wakamwambia, “Yuko
mwanamke mmoja huko Endori.”

[g]**28:1** 1Sam 29:1-2
[h]**28:2** Rum 12:9
[i]**28:3** 1Sam 25:1; 7:17; Kut 22:18; Isa 57:1, 2; Mdo 16:16, 19; Law 19:31; 20:27; Kum 18:10
[j]**28:4** Yos 19:18; 1Sam 31:1-3; 2Sam 1:6, 21; 21:12; Law 19:31; Kum 18:10-11; 2Fal 4:8
[k]**28:5** Kut 19:16; Ay 15:21; 18:11; Za 48:5, 6; 73:19; Isa 57:20; Dan 5:6
[l]**28:6** 1Sam 8:18; 14:37; Kum 13:3; Kut 28:30; Law 8:8; Eze 20:3; Amo 8:11; Mik 3:7; Hes 12:6; Mit 1:28; 1Nya 10:13-14
[m]6 Urimu na Thumimu maana yake ni Nuru na Kweli; vifaa hivi viliwekwa kwenye kifuko cha juu cha kisibau cha kuhani mkuu ili kujua mapenzi ya Mungu kwenye mambo ya kutatanisha.
[n]**28:7** 1Nya 10:13; Mdo 16:16; Yos 17:11; Za 83:10

8 [a]Hivyo Sauli akajigeuza kwa kuvaa
mavazi mengine, naye usiku akiwa
amefuatana na watu wawili wakaenda
kwa huyo mwanamke. Akamwambia,
“Nibashirie kwa uaguzi, unipandishie yule
nitakayekutajia.”
9 [b]Huyo mwanamke akamwambia,
“Wewe unajua lile alilofanya Mfalme
Sauli. Amewakatilia mbali waaguzi, wapiga
ramli wote na wachawi katika nchi. Mbona
umenitegea maisha yangu ili wapate
kuniua?”
10 Sauli akamwapia huyo mwanamke
kwa Jina la BWANA, akasema, “Kwa hakika
kama BWANA aishivyo, hutaadhibiwa kwa
ajili ya jambo hili.”
11 Ndipo yule mwanamke akauliza, “Je
unataka nikupandishie nani?”

Sauli akasema, “Nipandishie Samweli.”
12 [c]Yule mwanamke alipomwona
Samweli, alipiga yowe kwa sauti kuu, naye
akamuuliza Sauli, “Mbona umenidanganya?
Wewe ndiwe Sauli.”
13 [d]Mfalme akamwambia, “Usiogope.
Unaona nini?”

Yule mwanamke akasema, “Naona
mungu unapanda kutoka ardhini.”
14 [e]Sauli akamuuliza, “Ni mfano wa nini?”

Yule mwanamke akasema, “Ni mwanaume
mzee amevaa joho anayepanda.”

Ndipo Sauli akatambua kwamba ni
Samweli. Sauli akasujudu kifudifudi, uso
wake hadi ardhini.
15 [f]Samweli akamuuliza Sauli, “Kwa nini
unanitaabisha kwa kunipandisha juu?”

Sauli akasema, “Mimi ninasumbuka
sana, kwa maana Wafilisti wanapigana
vita dhidi yangu, naye Mungu ameniacha.
Hanijibu tena wala kwa njia ya manabii
wala kwa ndoto. Kwa hiyo nimekuita wewe
ili unijulishe la kufanya.”
16 Samweli akamuuliza, “Kwa nini
uniulize mimi, maadamu BWANA
amekuacha na kuwa adui yako?
17 [g]BWANA
ametenda lile alilotangulia kusema kupitia
kwangu. BWANA ameurarua ufalme kutoka
mikononi mwako, naye amempa mmoja wa
jirani zako, yaani Daudi.
18 [h]Kwa sababu
wewe hukumtii BWANA, wala hukumtimizia
ghadhabu yake kali juu ya Waamaleki,
BWANA amekutendea mambo haya leo.
19 [i]Zaidi ya hayo, BWANA atawatia Israeli
pamoja na wewe mikononi mwa Wafilisti,
na kesho wewe na wanao mtakuwa pamoja
nami. BWANA pia atalitia jeshi la Israeli
mikononi mwa Wafilisti.”
20 [j]Papo hapo Sauli akaanguka chini,
akajinyoosha, akiwa amejawa na hofu kwa
ajili ya maneno ya Samweli. Nguvu zake
zikamwishia kwa maana alikuwa hajala
chochote mchana ule wote na usiku.
21 [k]Yule mwanamke alipomwendea
Sauli na kumwona amepatwa na hofu,
akamwambia, “Tazama, mimi mtumishi
wako mwanamke nimekutii. Nimeweka
maisha yangu hatarini kwa kufanya kile
ulichoniagiza nifanye.
22 Sasa tafadhali
isikilize sauti ya mtumishi wako, uniruhusu
nikupatie chakula kidogo ule ili uwe na
nguvu za kurejea ulikotoka.”
23 [l]Akakataa, akisema, “Mimi sitaki kula.”

Lakini watumishi wake wakaungana
na yule mwanamke wakamsihi ale, naye
akakubali. Basi akainuka hapo chini,
akaketi juu ya kitanda.
24 [m]Yule mwanamke alikuwa na ndama
aliyenona hapo nyumbani, akamchinja
mara moja. Akachukua unga, akaukanda,
akatengeneza mkate usio chachu.
25 Ndipo
akamwandalia meza Sauli pamoja na watu
wake, nao wakala. Usiku ule ule wakainuka
na kwenda zao.

---

[a]**28:8** 1Fal 22:30; 2Nya 18:29; 35:22; 2Fal 1:3; Isa 8:19; 1Nya 10:13
[b]**28:9** Ay 18:10; Za 31:4; 69:22; Isa 8:14
[c]**28:12** Mwa 27:36; 1Fal 14:6; Isa 57:2; Ufu 14:13
[d]**28:13** Law 19:31; 2Nya 33:6
[e]**28:14** 1Sam 15:27; 24:8; 2The 2:10, 11
[f]**28:15** Amu 16:20; Kum 13:3; 1Sam 18:12
[g]**28:17** 1Sam 15:28
[h]**28:18** 1Sam 15:20; Kum 9:8; 1Sam 15:3; Mwa 14:7; 1Sam 14:48
[i]**28:19** 1Sam 31:2; 1Nya 8:33
[j]**28:20** 1Sam 25:37; Za 50:21
[k]**28:21** Amu 9:17; 12:3; Ay 13:14; 1Sam 19:5
[l]**28:23** 1Fal 21:4; 2Fal 5:13; Mwa 4:6; Mit 25:20, 21
[m]**28:24** Mwa 18:7, 8; Lk 15:23-30

*Akishi Amrudisha Daudi Huko Siklagi*

29 [a]Wafilisti wakakusanya majeshi
yao yote huko Afeki, nao Waisraeli
wakapiga kambi karibu na chemchemi
iliyoko Yezreeli. 2 [b]Watawala wa Wafilisti
walipokuwa wakipita pamoja na vikosi
vyao vya mamia na vya maelfu, Daudi na
watu wake walikuwa wakitembea huko
nyuma pamoja na Akishi. 3 [c]Majemadari
wa Wafilisti wakauliza, “Vipi kuhusu hawa
Waebrania?”

Akishi akajibu, “Huyu si Daudi,
aliyekuwa afisa wa Sauli mfalme wa Israeli?
Ameshakuwa pamoja nami kwa zaidi ya
mwaka, naye tangu alipomwacha Sauli hadi
sasa, sikuona kosa lolote kwake.”

4 [d]Lakini majemadari wa Wafilisti
wakamkasirikia na kusema, “Mrudishe
mtu huyu, apate kurudi mahali pale
ulipompangia. Haimpasi kufuatana
pamoja nasi vitani, asije akageuka, akawa
kinyume chetu vitani. Ni kwa njia ipi bora
zaidi angeweza kujipatia tena kibali kwa
bwana wake, isipokuwa kwa vichwa vya
watu wetu wenyewe? 5 [e]Je, huyu si ndiye
Daudi walioimba kumhusu katika ngoma
zao, wakisema:

“ ‘Sauli amewaua elfu zake,
naye Daudi makumi elfu yake’?”

6 [f]Basi Akishi akamwita Daudi na
kumwambia, “Kama vile BWANA aishivyo,
wewe umekuwa mtu mwaminifu, nami
ningependa utumike pamoja nami katika
jeshi. Tangu siku ile uliyofika kwangu hadi
sasa, sijaona kosa lolote kwako, lakini
hao watawala hawakukubali. 7 Rudi na
uende kwa amani; usifanye chochote cha
kuwakasirisha watawala wa Kifilisti.”

8 Daudi akamuuliza Akishi, “Lakini
mimi nimefanya nini? Je, umeona nini
kibaya juu ya mtumishi wako tangu siku
ile niliyokuja kwako hadi leo? Kwa nini
nisirudi na kupigana na adui za bwana
wangu mfalme?”

9 [g]Akishi akamjibu Daudi, “Mimi ninajua
ya kuwa wewe umekuwa wa kupendeza
machoni pangu kama vile malaika wa
Mungu. Lakini hao majemadari wa
Wafilisti wamesema, ‘Huyu haimpasi
kwenda vitani pamoja nasi.’ 10 [h]Sasa amka
mapema, pamoja na watumishi wa bwana
wako waliofuatana nawe, nanyi ondokeni
asubuhi mara kutakapopambazuka.”

11 [i]Hivyo Daudi na watu wake wakaamka
asubuhi na mapema, wakaenda zao kurudi
katika nchi ya Wafilisti, nao Wafilisti
wakapanda kwenda Yezreeli.

*Daudi Aangamiza Waamaleki*

30 [j]Daudi na watu wake wakafika
Siklagi siku ya tatu. Basi Waamaleki
walikuwa wamevamia Negebu na Siklagi.
Wakawa wameshambulia mji wa Siklagi
na kuuteketeza kwa moto, 2 [k]nao wakawa
wamewachukua mateka wanawake
pamoja na wote waliokuwamo humo,
vijana na wazee. Hawakuua yeyote, bali
waliwachukua wakaenda zao.

3 [l]Daudi na watu wake walipofika
Siklagi, wakakuta mji umeangamizwa
kwa moto na wake zao pamoja na wana
wao na binti zao wamechukuliwa mateka.
4 [m]Hivyo Daudi na watu wake wakapiga
yowe mpaka wakaishiwa na nguvu za
kulia. 5 [n]Wake wawili wa Daudi walikuwa
wametekwa: yaani Ahinoamu wa Yezreeli,
na Abigaili, mjane wa Nabali wa Karmeli.

---

[a]**29:1** 1Sam 28:1; 4:1; Yos 17:16; 1Fal 18:45; 21:1; 2Fal 9:30; Yer 50:5; Hos 1:4; 5:11; 2:22; Yos 12:18
[b]**29:2** 1Sam 28:2
[c]**29:3** 1Nya 12:19; 1Sam 27:7; Dan 6:5; Yn 19:6; 1Pet 3:16
[d]**29:4** 1Nya 12:19; 1Sam 14:21
[e]**29:5** 1Sam 18:7; 21:11
[f]**29:6** 1Sam 27:8-12; Hes 27:17; 2Sam 3:25; 2Fal 19:27; Za 121:8; Isa 37:28
[g]**29:9** 2Sam 14:17, 20; 19:27
[h]**29:10** 1Nya 12:19
[i]**29:11** Za 37:23; 73:2; Mit 16:9; 20:24; Isa 30:21; Yer 10:23; 1Kor 10:23; 10:13; 2Sam 4:4
[j]**30:1** 1Sam 27:6-8; 29:4, 11; 15:7; Kut 17:8-16; Hes 24:20; Kum 25:17, 19; 1Nya 4:43; Eze 25:15
[k]**30:2** Ay 38:11; Za 76:10; 89:9; Isa 27:8; Hab 3:2
[l]**30:3** Mwa 31:26
[m]**30:4** Mwa 27:38; Hes 14:1
[n]**30:5** 1Sam 25:43; 2Sam 2:2

6 [a]Daudi alihuzunika sana kwa sababu watu
walikuwa wakisemezana juu ya kumpiga
kwa mawe. Kila mmoja alikuwa na uchungu
rohoni kwa sababu ya wanawe na binti
zake. Lakini Daudi akajitia nguvu katika
BWANA, Mungu wake.
7 [b]Kisha Daudi akamwambia kuhani
Abiathari mwana wa Ahimeleki, "Niletee
kisibau." Abiathari akamletea, 8 [c]naye Daudi
akamuuliza BWANA, "Je, nifuatie kundi hili
la wavamizi? Je, nitawapata?"
BWANA akajibu, "Wafuatie. Hakika
utawapata na utafanikiwa kuwaokoa."
9 [d]Daudi pamoja na watu wake 600
wakafika kwenye Bonde la Besori, mahali
ambapo wengine waliachwa nyuma, 10 kwa
kuwa watu 200 walikuwa wamechoka sana
kuweza kuvuka hilo bonde. Lakini Daudi
pamoja na watu 400 wakaendelea kufuatia.
11 [e]Wakamkuta Mmisri katika shamba
fulani, nao wakamleta kwa Daudi. Wakampa
huyo Mmisri maji ya kunywa na chakula;
12 [f]kipande cha andazi la tini na andazi la
zabibu zilizokaushwa. Akala naye akapata
nguvu, kwa kuwa hakuwa amekula chakula
chochote wala kunywa maji kwa siku tatu
usiku na mchana.
13 [g]Daudi akamuuliza, "Wewe ni wa nani,
na umetoka wapi?"
Akajibu, "Mimi ni Mmisri, mtumwa wa
Mwamaleki. Bwana wangu alinitelekeza
nilipougua siku tatu zilizopita. 14 [h]Tulivamia
Negebu ya Wakerethi, na nchi ya Yuda, na
Negebu ya Kalebu. Nasi tulichoma moto
Siklagi."
15 [i]Daudi akamuuliza, "Je, unaweza
kuniongoza kufikia kundi hili la uvamizi?"
Akajibu, "Niapie mbele ya Mungu
kwamba hutaniua wala kunikabidhi
mikononi mwa bwana wangu, nami
nitakupeleka hadi waliko."
16 [jk]Akamwongoza Daudi mpaka mahali
walipokuwa, nao walikuwa wametawanyika
eneo lote, wakila, wakinywa na wakifanya
karamu kwa sababu ya nyara nyingi
walizochukua kutoka nchi ya Wafilisti
na kutoka Yuda. 17 [lm]Daudi akapigana nao
kuanzia machweo ya jua hadi kesho yake
jioni, na hakuna yeyote miongoni mwao
aliyetoroka, isipokuwa vijana wanaume 400
waliopanda ngamia na kutoroka. 18 [n]Daudi
akarudisha kila kitu Waamaleki walikuwa
wamechukua, pamoja na wake zake wawili.
19 Hakuna chochote kilichopotea: kijana
au mzee, mvulana au msichana, nyara
au kitu kingine chochote walichokuwa
wamechukua. Daudi akarudisha kila kitu.
20 Akachukua makundi yote ya kondoo,
mbuzi na ng'ombe, nao watu wake
wakawaswaga wanyama hao mbele ya
wanyama wengine wa kufugwa, wakisema,
"Hizi ni nyara za Daudi."
21 [o]Kisha Daudi akafika kwa wale watu
200 waliokuwa wamechoka sana kumfuata
na ambao waliachwa nyuma kwenye Bonde
la Besori. Wakatoka kwenda kumlaki Daudi
na wale watu aliokuwa nao. Daudi na watu
wake walipowakaribia, akawasalimu.
22 [p]Lakini watu wote waovu na wakorofi
miongoni mwa wafuasi wa Daudi wakasema,
"Kwa sababu hawakwenda pamoja nasi,
hatutagawana nao nyara tulizorudisha.
Lakini, kila mtu aweza kuchukua mkewe
na watoto wake na kuondoka."
23 Daudi akajibu, "La hasha, ndugu
zangu, kamwe hamwezi kufanya hivyo kwa
kile ambacho BWANA ametupatia. Yeye
ametulinda na kuweka mikononi mwetu
majeshi yale yaliyokuja kupigana dhidi

[a]**30:6** Kut 17:4; Yn 8:59; Za 27:14; Rut 1:13; Rum 4:20; Amu 18:25; 2Sam 17:8; Za 17:8; Yer 17:7, 17; Yoe 3:16; Rum 4:20
[b]**30:7** 1Sam 22:20; 2:28; 23:9
[c]**30:8** 1Sam 23:2; Mwa 14:16; Kut 2:17
[d]**30:9** 1Sam 27:2
[e]**30:11** Za 11:2; Mit 3:5, 6
[f]**30:12** Amu 15:19; 1Sam 14:27
[g]**30:13** 1Sam 14:48
[h]**30:14** 2Sam 8:18; 15:18; 20:2, 23; 1Fal 1:38, 44; 1Nya 18:17; Sef 2:5; Yos 14:13; 15:13
[i]**30:15** Kum 23:15
[j]**30:16** Lk 12:19; Yos 22:8
[k]**30:16** Kut 32:6; 1Sam 25:36-38; 2Sam 13:28; Dan 5:1-4; Lk 12:19-20; 21:34; 1The 5:3; Ufu 11:10, 13
[l]**30:17** 1Sam 11:11; 2Sam 1:1; 15:3; 1:8
[m]**30:17** Ay 20:5
[n]**30:18** Mwa 14:16; Za 34:9
[o]**30:21** Amu 18:9
[p]**30:22** Kum 13:13; Amu 19:22; 1Sam 22:2; 25:17; 1Fal 21:10

yetu. 24 [a]Ni nani atasikiliza yale mnayosema?
Fungu la mtu aliyekaa na vyombo litakuwa
sawa na la yule aliyekwenda vitani. Wote
watashiriki sawa.” 25 Daudi akafanya hili
liwe amri na agizo kwa Israeli kutoka siku
ile hata leo.

26 [b]Daudi alipofika Siklagi, akatuma
baadhi ya nyara kwa wazee wa Yuda,
waliokuwa rafiki zake, akasema, “Tazama,
hapa kuna zawadi kwa ajili yenu kutoka
nyara za adui za BWANA.”

27 [c]Akazituma kwa wale waliokuwa
Betheli, Ramoth-Negebu na Yatiri; 28 [d]kwa
wale walioko Aroeri, Sifmothi, Eshtemoa
29 [e]na Rakali; kwa wale waliokuwa katika
miji ya Wayerameeli na ya Wakeni; 30 [f]na
kwa wale walioko Horma, Bori-Ashani,
Athaki, 31 [g]na kwa wakazi wa Hebroni; na
kwa wale waliokuwa mahali pengine pote
ambako Daudi na watu wake walitembelea.

*Sauli Ajiua*

### (1 Nyakati 10:1-12)

31 [h]Basi Wafilisti wakapigana na Israeli.
Waisraeli wakawakimbia, na wengi
wakauawa katika Mlima Gilboa. 2 [i]Wafilisti
wakawafuatia kwa bidii Sauli na wanawe,
wakawaua Yonathani, Abinadabu na Malki-
Shua. 3 [j]Mapigano yakawa makali sana
kumzunguka Sauli, nao wapiga upinde
wakampata na kumjeruhi vibaya.

4 [k]Sauli akamwambia mbeba silaha
wake, “Futa upanga wako unichome nao, la
sivyo hawa watu wasiotahiriwa watakuja
wanichome na kunidhalilisha.”

Lakini mbeba silaha wake akaogopa
sana wala hakuweza kufanya hivyo.
Kwa hiyo Sauli akachukua upanga wake
mwenyewe na kuuangukia. 5 Mchukua
silaha wake alipoona Sauli amekufa, naye
pia akaangukia upanga wake akafa pamoja
naye. 6 [l]Basi Sauli, wanawe watatu, mbeba
silaha wake na watu wake wote wakafa
pamoja siku ile ile.

7 Waisraeli waliokuwa kandokando ya
bonde na wale waliokuwa ng’ambo ya
Yordani walipoona kuwa jeshi la Waisraeli
limekimbia na kwamba Sauli na wanawe
wamekufa, wakaacha miji yao na kukimbia.
Nao Wafilisti wakaja na kukaa humo.

8 [m]Kesho yake Wafilisti walipokuja
kuwavua maiti silaha, walimkuta Sauli
na wanawe watatu wameanguka katika
Mlima Gilboa. 9 [n]Wakamkata Sauli kichwa
na kumvua silaha zake, nao wakatuma
wajumbe katika nchi yote ya Wafilisti
kutangaza habari katika hekalu la
sanamu zao na miongoni mwa watu wao.
10 [o]Wakaweka silaha zake katika hekalu la
Maashtorethi, na kukifunga kiwiliwili chake
katika ukuta wa Beth-Shani.

11 [p]Watu wa Yabeshi-Gileadi waliposikia
yale Wafilisti walichomfanyia Sauli,
12 [q]mashujaa wao wote wakaenda usiku hadi
Beth-Shani. Wakauchukua mwili wa Sauli
na miili ya wanawe kutoka kwenye ukuta
wa Beth-Shani na kurudi hadi Yabeshi,
mahali ambapo waliiteketeza kwa moto.
13 [r]Kisha wakachukua mifupa yao na kuizika
chini ya mti wa mkwaju huko Yabeshi, nao
wakafunga siku saba.

---

[a]**30:24** Hes 31:27; Amu 5:30; Yos 22:8
[b]**30:26** Mwa 33:11
[c]**30:27** Yos 7:2; 10:40; 15:48; 19:8; Mwa 12:8; Yos 7:2; 10:40
[d]**30:28** Hes 32:34; Yos 13:16; 1Nya 27:27; Yos 15:50
[e]**30:29** 1Sam 27:10; Amu 1:16; 1Sam 15:6
[f]**30:30** Hes 13:22; Yos 10:36; 14:13; 2Sam 2:1-4
[g]**30:31** Hes 13:22; Yos 10:36; 14:13; 2Sam 2:1-4
[h]**31:1** 1Sam 28:4; 1Nya 10:1-12; 1Sam 29:1; 1Nya 8:33
[i]**31:2** 1Sam 28:19; 18:1; 14:49; 1Nya 8:33
[j]**31:3** 1Sam 28:4; 2Sam 1:6
[k]**31:4** Amu 9:54; Mwa 34:14; 1Sam 14:6; 2Sam 1:6, 10
[l]**31:6** 1Sam 26:10; 12:25; 1Nya 10:6; Rum 6:23
[m]**31:8** 2Sam 1:20
[n]**31:9** 1Sam 1:20; 4:4; Amu 16:24
[o]**31:10** Amu 2:12-13; 1Sam 7:3; Yos 17:11; 2Sam 21:12; 1Sam 21:9; Amu 1:27
[p]**31:11** Amu 21:8; 1Sam 11:1
[q]**31:12** Za 76:5; Mwa 38:24; Amo 6:10; 2Nya 16:14; 1Sam 11:1-11; 2Sam 2:4-7; Yer 34:5; Amo 6:10
[r]**31:13** 2Sam 21:12-14; Mwa 21:33; 2Sam 3:35; 12:19-23; 1:12; Mwa 50:10; 1Sam 22:6; Mwa 50:10; Ay 2:13

# 2 SAMWELI

*Daudi Afahamishwa Kifo Cha Sauli*

1 [a]Baada ya kifo cha Sauli, Daudi alipokuwa
amerudi kutoka kuwashinda Waamaleki,
Daudi alikaa siku mbili huko Siklagi.
2 [b]Siku ya tatu akaja mtu mwenye nguo
zilizoraruka na mavumbi kichwani mwake
kutoka kwenye kambi ya Sauli. Alipomjia
Daudi, akajitupa chini ili kumpa heshima.
3 Daudi akamuuliza, “Wewe umetoka
wapi?”

Akamjibu, “Nimetoroka kutoka kambi
ya Waisraeli.”

4 [c]Daudi akamuuliza, “Ni nini
kilichotokea? Niambie.”

Akasema, “Watu walikimbia kutoka
vitani. Wengi wao walianguka na kufa. Naye
Sauli na Yonathani mwanawe wamekufa.”

5 Ndipo Daudi akamwambia huyo kijana
aliyemletea taarifa, “Je, umefahamuje
kwamba Sauli na Yonathani mwanawe
wamekufa?”

6 [d]Yule kijana akasema, “Nilijipata huko
Mlima Gilboa, naye Sauli alikuwa huko
akiegemea mkuki wake, na magari ya vita
na wapanda farasi wa upande wa adui
wakawa wamemkaribia sana. 7 Alipogeuka
na kuniona, akaniita, nami nikasema, ‘Je,
nifanye nini?’

8 [e]“Akaniuliza, ‘Wewe ni nani?’

“Nikamjibu, ‘Mimi ni Mwamaleki.’

9 [f]“Kisha akaniambia, ‘Nikaribie mimi na
uniue! Niko katika maumivu makali ya kifo,
lakini bado ningali hai.’

10 [g]“Kwa hiyo nikamkaribia nikamuua,
kwa sababu nilijua kwamba baada ya
kuanguka hangeweza kupona. Nami
nikachukua lile taji lililokuwa kichwani
mwake na utepe uliokuwa mkononi mwake
nami nimevileta hapa kwa bwana wangu.”

11 [h]Ndipo Daudi pamoja na watu wote
waliokuwa pamoja naye wakazishika nguo
zao na kuzirarua. 12 Wakaomboleza, wakalia
pia na kufunga mpaka jioni kwa ajili ya
Sauli na Yonathani mwanawe, kwa ajili ya
jeshi la BWANA na nyumba ya Israeli, kwa
sababu wameanguka kwa upanga.

13 [i]Daudi akamwambia yule kijana
aliyemletea taarifa, “Wewe ni mwenyeji
wa wapi?”

Akamjibu, “Mimi ni mwana wa mgeni,
Mwamaleki.”

14 [j]Daudi akamuuliza, “Kwa nini
hukuogopa kuinua mkono wako ili
kumwangamiza mpakwa mafuta wa
BWANA?”

15 [k]Kisha Daudi akamwita mmoja wa watu
wake na kumwambia, “Nenda ukamuue!”
Kwa hiyo akampiga, naye akafa. 16 [l]Kwa
maana Daudi alikuwa amemwambia, “Damu
yako iwe juu ya kichwa chako mwenyewe.
Kinywa chako mwenyewe kimeshuhudia
dhidi yako uliposema, ‘Nilimuua mpakwa
mafuta wa BWANA.’ ”

*Ombolezo La Daudi Kwa Ajili Ya Sauli Na Yonathani*

17 [m]Daudi akafanya maombolezo haya
kuhusu Sauli na Yonathani mwanawe,
18 [n]naye akaagiza kwamba watu wa Yuda
wafundishwe ombolezo hili la upinde
(ambalo limeandikwa katika Kitabu cha
Yashari):

[a]**1:1** 1Sam 26:10; 1Nya 10:13; Yos 22:8; 1Sam 30:17; Mwa 14:7; Hes 13:29; 1Sam 11:11; 1Fal 20:29-30
[b]**1:2** 2Sam 4:10; Ay 2:12; Eze 27:30; 1Sam 20:41; Mwa 37:7; 37:29; 44:13; Hes 14:6; Yos 7:6; Ay 1:20; Mdo 14:14
[c]**1:4** 1Sam 4:16
[d]**1:6** 1Sam 28:4; 31:2-4; 1Nya 10:1-3
[e]**1:8** 1Sam 15:2; 27:8; 30:13, 17
[f]**1:9** Amu 9:54
[g]**1:10** Amu 9:54; 2Fal 11:12
[h]**1:11** Mwa 37:29; Hes 14:6; Yos 7:6; 2Sam 3:31; 13:31; Ezr 9:3; 2Nya 34:27; Yoe 2:13
[i]**1:13** 1Sam 14:48
[j]**1:14** 1Sam 12:3; 26:9; 24:6; Hes 12:8; Za 105:15
[k]**1:15** 2Sam 4:10-12; Amu 8:20; 1Sam 22:17-18; 1Fal 2:25, 34, 46
[l]**1:16** Law 20:9; Mt 27; 24:25; Mdo 18:6; 1Sam 26:9; Lk 19:22
[m]**1:17** Mwa 50:10; Eze 32:2; 2Nya 35:25
[n]**1:18** Yos 10:13; 1Sam 31:3

19 [a]"Walio fahari yako, ee Israeli,
wameuawa juu ya mahali
pako palipoinuka.
Jinsi wenye nguvu walivyoanguka!

20 [b]"Msilisimulie hili katika Gathi,
msilitangaze hili katika
barabara za Ashkeloni,
binti za Wafilisti wasije wakafurahia,
binti za hao wasiotahiriwa
wasije wakashangilia.

21 [c]"Enyi milima ya Gilboa,
msipate umande wala mvua,
wala mashamba yazaayo sadaka
ya nafaka.
Kwa maana huko ndiko ngao ya
mwenye nguvu iliponajisiwa,
ngao ya Sauli haitapakwa tena
mafuta.
22 [d]Kutokana na damu ya waliouawa,
kutokana na miili ya wenye
nguvu,
ule upinde wa Yonathani
haukugeuka nyuma.
Upanga wa Sauli haukurudi bure.

23 [e]"Sauli na Yonathani,
maishani walipendwa na
kuneemeka,
na katika kifo hawakutengana.
Walikuwa wepesi kuliko tai,
walikuwa na nguvu kuliko simba.

24 [f]"Enyi binti za Israeli,
lieni kwa ajili ya Sauli,
ambaye aliwavika nguo
nyekundu na maridadi,
ambaye aliremba mavazi yenu
kwa mapambo ya dhahabu.

25 "Tazama jinsi mashujaa
walivyoanguka vitani!
Yonathani ameuawa
mahali pako palipoinuka.
26 [g]Nahuzunika kwa ajili yako,
Yonathani ndugu yangu,
kwangu ulikuwa mpendwa sana.
Upendo wako kwangu ulikuwa wa
ajabu,
wa ajabu zaidi kuliko ule wa
wanawake.

27 [h]"Tazama jinsi mashujaa
walivyoanguka!
Silaha za vita zimeangamia!"

*Daudi Atiwa Mafuta Kuwa Mfalme Wa Yuda*

2 [i]Ikawa baada ya mambo haya, Daudi
akamuuliza BWANA, "Je, nipande
kwenda katika mojawapo ya miji ya Yuda?"
BWANA akasema, "Panda."
Daudi akauliza, "Je, niende wapi?"
BWANA akajibu, "Nenda Hebroni."
2 [j]Basi Daudi akakwea kwenda huko
pamoja na wake zake wawili, Ahinoamu
wa Yezreeli na Abigaili, mjane wa Nabali
wa Karmeli. 3 [k]Pia Daudi akawachukua watu
waliokuwa pamoja naye, kila mmoja na
jamaa yake, nao wakaishi huko Hebroni na
miji yake. 4 [l]Ndipo watu wa Yuda wakaja
Hebroni, huko wakamtia Daudi mafuta awe
mfalme juu ya nyumba ya Yuda.
Daudi alipoambiwa kuwa ni watu
wa Yabeshi-Gileadi waliomzika Sauli,
5 [m]akatuma wajumbe kwa watu wa Yabeshi-
Gileadi kuwaambia, "BWANA awabariki
kwa kuonyesha wema huu kwa kumzika

---

[a]**1:19** 2Sam 23:8; Za 29:1; 45:3; 2Sam 3:38
[b]**1:20** Mik 1:10; Yos 13:3; 1Sam 31:8; 18:6; Amu 16:23; Kut 15:20; Amu 11:34
[c]**1:21** Mwa 27:28; Isa 18:4; Kum 11:17; 1Fal 8:35; 17:1; 18:1; 2Nya 6:26; Ay 36:27; 38:28; Za 65:10; 147:8; Isa 5:6; Yer 5:24; 14:4; 12:4; Eze 31:5; Isa 21:5
[d]**1:22** Isa 34:3, 7; 49:26; Kum 32:42; 1Sam 18:4
[e]**1:23** Kum 28:49; Amu 14:18; Yer 4:13
[f]**1:24** Amu 5:30
[g]**1:26** Yer 22:18; 34:5; 1Sam 20:42; 18:1; 19:2; 20:17
[h]**1:27** 1Sam 2:4
[i]**2:1** 1Sam 23:2, 11-12; Mwa 13:18; 23:19; 1Sam 30:31; Hes 27:21; 1Sam 23:2-9; 1Fal 2:11
[j]**2:2** 1Sam 25:42-43; 30:5
[k]**2:3** 1Sam 27:2; 1Nya 12:22; Mwa 13:18; 23:2; 37:14
[l]**2:4** 1Sam 30:31; 2:35; 2Sam 5:3-5; 1Nya 12:23-40; Amu 21:8; 1Sam 11:1; 31:11-13
[m]**2:5** Amu 17:2; 1Sam 23:21; 2Tim 1:16; Za 115:15

Sauli bwana wenu. 6 [a]Sasa BWANA na
awaonyeshe wema na uaminifu, nami pia
nitawaonyesha wema ule ule kwa kuwa
mmefanya jambo hili. 7 [b]Sasa basi, kuweni
hodari na mashujaa, kwa maana bwana
wenu Sauli amekufa, nayo nyumba ya Yuda
imenitia mafuta niwe mfalme juu yao."

*Vita Kati Ya Nyumba Ya Daudi Na Sauli*

8 [c]Wakati huo Abneri mwana wa Neri,
jemadari wa jeshi la Sauli, alikuwa
amemchukua Ish-Boshethi mwana wa Sauli
na kumleta hadi Mahanaimu. 9 [d]Akamweka
awe mfalme juu ya nchi ya Gileadi,
Waasheri,[e] Yezreeli, Efraimu, Benyamini
na Israeli yote.
10 Ish-Boshethi[f] mwana wa Sauli alikuwa
na umri wa miaka arobaini alipoanza
kutawala Israeli, naye akatawala miaka
miwili. Hata hivyo, nyumba ya Yuda
ikamfuata Daudi. 11 [g]Muda ambao Daudi
alikuwa mfalme juu ya nyumba ya Yuda
huko Hebroni ilikuwa miaka saba na miezi
sita.
12 [h]Abneri mwana wa Neri, pamoja na
watu wa Ish-Boshethi mwana wa Sauli,
wakatoka Mahanaimu kwenda Gibeoni.
13 [i]Yoabu mwana wa Seruya na watu wa
Daudi wakatoka na kukutana nao kwenye
bwawa la Gibeoni. Kikundi kimoja kiliketi
upande mmoja wa bwawa, na kikundi
kingine upande wa pili.
14 [j]Ndipo Abneri akamwambia Yoabu,
"Tuwaweke baadhi ya vijana wasimame
na wapigane ana kwa ana mbele yetu."
Yoabu akasema, "Sawa, na wafanye
hivyo."
15 Kwa hiyo vijana wakasimama,
wakahesabiwa: watu wa Benyamini na
wa Ish-Boshethi mwana wa Sauli kumi
na wawili, na upande wa Daudi kumi na
wawili. 16 [k]Kisha kila mtu akakamatana na
mpinzani wake kichwani na kuchomana
kwa upanga, nao wakaanguka chini
pamoja. Kwa hiyo mahali pale katika
Gibeoni pakaitwa Helkath-Hasurimu.[l]
17 [m]Siku hiyo vita vilikuwa vikali
sana, naye Abneri na watu wa Israeli
wakashindwa na watu wa Daudi.
18 [n]Wana watatu wa Seruya walikuwako
huko: nao ni Yoabu, Abishai na Asaheli.
Basi huyo Asaheli alikuwa na mbio kama
paa. 19 Asaheli akamfukuza Abneri, pasipo
kugeuka kulia wala kushoto wakati
akimfuata. 20 Abneri akaangalia nyuma na
kumuuliza, "Ni wewe, Asaheli?"
Akamjibu, "Ndiyo."
21 [o]Ndipo Abneri akamwambia, "Geuka
upande wa kulia au kushoto. Mchukue
mmoja wa vijana wa kiume na umvue silaha
zake." Lakini Asaheli hakuacha kumfukuza.
22 [p]Abneri akamwonya tena Asaheli
akimwambia, "Acha kunifukuza! Kwa nini
nikuue? Je, nitawezaje kumtazama ndugu
yako Yoabu usoni?"
23 [q]Lakini Asaheli alikataa kuacha
kumfuatia, kwa hiyo Abneri akamchoma
Asaheli tumboni kwa ncha butu ya
mkuki wake, mkuki ukamtoboa ukatokea
mgongoni mwake. Akaanguka na kufa papo
hapo. Ikawa kila mtu alisimama alipofika
mahali pale Asaheli alipoanguka na kufa.
24 [r]Lakini Yoabu na Abishai walimfuata
Abneri, na jua lilipokuwa linatua, wakafika

[a]**2:6** Kut 34:6; 2Tim 1:16; Mt 5:44
[b]**2:7** Yos 1:6; Amu 5:21
[c]**2:8** 1Sam 14:50; 2Sam 3:27; 4:5; 1Nya 8:33; 9:36-39; Mwa 32:2; 1Sam 17:55; 2Sam 17:27
[d]**2:9** Hes 32:26; Yos 19:24-31; 1Nya 12:29; Amu 1:32
[e]9 Waasheri hapa ni kabila moja la Israeli.
[f]10 Ish-Boshethi maana yake Mtu wa Aibu, pia anaitwa Esh-Baali maana yake Mtu wa Baali (1Nya 8:33; 9:39).
[g]**2:11** 2Sam 5:5
[h]**2:12** Yos 9:3; 18:25; Isa 28:21
[i]**2:13** 2Sam 8:16; 19:13; 1Fal 1:17; 1Nya 2:16; 22:6; 27:34; Yer 41:12
[j]**2:14** Mit 10:23; 13:10
[k]**2:16** Amu 3:21
[l]16 Helkath-Hasurimu maana yake Uwanja wa Mapambano.
[m]**2:17** 2Sam 3:1; 1Sam 17:8; 1Fal 20:11
[n]**2:18** 2Sam 3:39; 16:10; 19:22; 3:30; 10:7; 11:1; 14:1; 18:14; 20:8; 24:3; 1Fal 1:7; 2:5, 34; 1Sam 26:6; 2Sam 23:24; 2Nya 2:16; 1Nya 11:26; 27:1; 12:8; Za 6:5; Wim 2:9
[o]**2:21** 1Sam 17:42
[p]**2:22** 2Sam 3:27
[q]**2:23** 2Sam 3:27; 4:6; 20:17
[r]**2:24** Yos 9:3; 10:2

kwenye kilima cha Ama, karibu na Gia
kwenye njia ya kuelekea kwenye nyika
ya Gibeoni. 25 Ndipo watu wa kabila la
Benyamini wakakusanyika tena nyuma ya
Abneri. Wakaunda kikosi na kujiimarisha
juu ya kilima.
26 [a]Abneri akamwita Yoabu, akamwambia,
“Je, ni lazima upanga uendelee kuangamiza
milele? Hutambui kwamba jambo hili
litaishia katika uchungu? Utaacha
kuwaagiza watu wako waache kuwafuatilia
ndugu zao hata lini?”
27 [b]Yoabu akajibu, “Hakika kama
aishivyo Mungu, kama hukusema, hawa
watu wangeendelea kuwafuatia ndugu zao
mpaka asubuhi.”
28 [c]Basi Yoabu akapiga tarumbeta, nao
watu wote wakasimama, hawakuwafuata
Israeli tena, wala hawakuwapiga tena.
29 [d]Usiku ule wote Abneri na watu wake
wakatembea kupitia Araba. Wakavuka Mto
Yordani, wakaendelea wakipitia nchi yote
ya Bithroni wakafika Mahanaimu.
30 Basi Yoabu akarudi kutoka kumfuatia
Abneri, na kuwakusanya watu wake wote.
Pamoja na Asaheli, watu kumi na tisa wa
Daudi walikuwa wamepotea. 31 Lakini watu
wa Daudi walikuwa wamewaua watu wa
kabila la Benyamini 360 waliokuwa pamoja
na Abneri. 32 [e]Wakamchukua Asaheli,
wakamzika katika kaburi la baba yake huko
Bethlehemu. Kisha Yoabu na watu wake
wakatembea usiku kucha na kufika huko
Hebroni wakati wa mapambazuko.

3 [f]Vita kati ya nyumba ya Sauli na nyumba
ya Daudi vilidumu kwa muda mrefu.
Daudi akaendelea kuwa imara zaidi na
zaidi, wakati nyumba ya Sauli iliendelea
kudhoofika zaidi na zaidi.

2 [g]Wana walizaliwa kwa Daudi huko
Hebroni:
Mzaliwa wake wa kwanza alikuwa
Amnoni mwana wa Ahinoamu wa
Yezreeli;
3 [h]mzaliwa wake wa pili alikuwa
Danieli[i] mwana wa Abigaili,
mjane wa Nabali wa Karmeli;
wa tatu, Absalomu mwana wa
Maaka, binti Talmai mfalme wa
Geshuri;
4 [j]wa nne, Adoniya mwana wa
Hagithi;
wa tano, Shefatia mwana wa
Abitali;
5 wa sita, Ithreamu mwana wa Egla,
mkewe Daudi.
Hawa ndio waliozaliwa kwa Daudi
huko Hebroni.

*Abneri Anamwendea Daudi*

6 [k]Wakati wa vita kati ya nyumba ya
Sauli na nyumba ya Daudi, Abneri alikuwa
anajiimarisha katika nafasi yake kwenye
nyumba ya Sauli. 7 [l]Basi Sauli alikuwa
amekuwa na suria, jina lake Rispa binti
wa Aiya. Naye Ish-Boshethi akamwambia
Abneri, “Kwa nini umekutana kimwili na
suria wa baba yangu?”
8 [m]Abneri akakasirika sana kwa sababu
ya kile Ish-Boshethi alichosema, naye
akamjibu, “Je, mimi ni kichwa cha mbwa,
kwa upande wa Yuda? Siku hii ya leo
mimi ni mtiifu kwa nyumba ya baba yako
Sauli, kwa jamaa yake na rafiki zake.
Sijakukabidhi kwa Daudi, lakini bado
unanilaumu kwa kosa la kuhusika na huyu
mwanamke! 9 [n]Mungu na amshughulikie

[a]**2:26** Kum 32:42; Yer 46:10, 14; Nah 2:13; 3:15; Ay 18:2; 19:2; Za 4:2; Mdo 7:16
[b]**2:27** Mit 17:14; 20:18; Lk 14:31-32
[c]**2:28** 2Sam 18:16; 20:23; Amu 3:27
[d]**2:29** Kum 3:17; Mwa 32:2; Wim 2:17; Yos 21:38; 2Sam 17:24
[e]**2:32** Mwa 49:29; 47:29-30; Amu 8:32; 2Sam 17:24
[f]**3:1** 1Fal 14:30; 2Sam 5:12; 2:17; 22:44; Es 9:4; Za 46:9; Isa 2:4; Mik 4:3; Mt 10:35-36; Gal 5:17; Efe 6:12
[g]**3:2** 2Sam 13:1; 1Sam 25:43; 1Nya 3:1-3
[h]**3:3** 1Sam 25:42; 2Sam 13:1, 28, 37; 14:32; 15:8
[i]3 Jina lingine lake ni Kileabu.
[j]**3:4** 1Fal 1:5-11; 2:13, 22
[k]**3:6** 1Sam 14:50; 2Sam 2:8-9; 2Nya 25:8
[l]**3:7** Mwa 22:24; 2Sam 16:21-22; 1Fal 1:3; 2Sam 21:8-11
[m]**3:8** 1Sam 17:43; 2Sam 9:8; 16:9; 8; 13; 1Sam 24:14; Kut 23:18
[n]**3:9** 1Sam 15:28; Rut 1:17; 1Fal 19:2; 1Sam 16:12; 1Nya 12:23; Za 78:70; 89:19-20; Mdo 13:22

Abneri, tena kwa ukali, ikiwa sitafanya kwa
ajili ya Daudi kile BWANA alichomwahidi
kwa kiapo, 10 [a]na kuuhamisha ufalme kutoka
kwenye nyumba ya Sauli na kuimarisha kiti
cha ufalme cha Daudi juu ya Israeli na Yuda
kuanzia Dani mpaka Beer-Sheba." 11 Ish-
Boshethi hakuthubutu kusema neno jingine
kwa Abneri, kwa sababu alimwogopa
Abneri.

12 Ndipo Abneri akatuma wajumbe kwa
niaba yake kwa Daudi, kumwambia, "Nchi
hii ni ya nani? Fanya mapatano na mimi,
nami nitakusaidia kuiweka Israeli yote juu
yako."

13 [b]Daudi akasema, "Vyema, nitafanya
mapatano nawe. Lakini nahitaji jambo
moja kwako: Usije mbele yangu mpaka
umemleta Mikali binti Sauli wakati
utakapokuja kuniona." 14 [c]Kisha Daudi
akapeleka wajumbe kwa Ish-Boshethi
mwana wa Sauli, kudai, "Nipe Mikali mke
wangu, ambaye nilimposa mwenyewe kwa
mahari ya magovi 100 ya Wafilisti."

15 [d]Kwa hiyo Ish-Boshethi akatoa amri
kwamba Mikali achukuliwe kutoka kwa
Paltieli mumewe, mwana wa Laishi. 16 [e]Hata
hivyo, mumewe alikwenda pamoja naye,
akilia nyuma ya mkewe njia yote hadi
Bahurimu. Ndipo Abneri akamwambia
Paltieli, "Rudi nyumbani!" Kwa hiyo
akarudi.

17 [f]Abneri akafanya shauri pamoja na
wazee wa Israeli, akasema, "Muda mrefu
mmetaka kumfanya Daudi mfalme wenu.
18 [g]Sasa fanyeni hivyo! Kwa maana BWANA
alimwahidi Daudi akisema, 'Kwa kupitia
Daudi mtumishi wangu nitawaokoa watu
wangu Israeli kutoka mikononi mwa
Wafilisti na kutoka mikononi mwa adui
zako wote.' "

19 [h]Pia Abneri mwenyewe akazungumza
na kabila la Benyamini. Kisha akaenda
mpaka Hebroni kumwambia Daudi kila
kitu ambacho Israeli na nyumba yote ya
Benyamini walichotaka kufanya. 20 [i]Wakati
Abneri aliyekuwa na watu ishirini
pamoja naye, alipokuja kwa Daudi huko
Hebroni, Daudi akamwandalia karamu
pamoja na watu wake. 21 [j]Ndipo Abneri
akamwambia Daudi, "Niache niende
mara moja nikakusanye Israeli yote kwa
ajili ya mfalme bwana wangu, ili waweze
kufanya mapatano na wewe, ili kwamba
uweze kutawala juu ya yote yale ambayo
moyo wako unaonea shauku." Basi Daudi
akamuaga Abneri, naye akaenda kwa
amani.

*Yoabu Amuua Abneri*

22 Wakati huo huo, watu wa Daudi
na Yoabu walirudi kutoka kwenye
kushambulia, nao wakarudi na nyara
nyingi mno. Lakini Abneri hakuwa tena
pamoja na Daudi huko Hebroni, kwa
sababu Daudi alikuwa amemruhusu aende
zake, naye akaenda kwa amani. 23 Yoabu
na askari wote aliokuwa nao walipowasili,
aliambiwa kwamba Abneri mwana wa Neri
alikuwa amekuja kwa mfalme na kwamba
mfalme alikuwa amemruhusu aende zake,
na kwamba alikwisha ondoka kwa amani.

24 Basi Yoabu alikwenda kwa mfalme na
kumwambia, "Ni nini hiki ulichofanya?
Tazama, Abneri alikuja kwako. Kwa nini
ukamwacha aende? Sasa amekwenda!
25 [k]Wajua Abneri mwana wa Neri alikuja
kukudanganya na kuchunguza nyendo zako
na kupata kila kitu unachokifanya."

26 Ndipo Yoabu akamwacha Daudi na
kutuma wajumbe wamfuate Abneri, nao
wakamrudisha kutoka kisima cha Sira.
Lakini Daudi hakufahamu jambo hili.
27 [l]Basi Abneri aliporudi Hebroni, Yoabu
akamchukua kando ndani ya lango, kama

---

[a]**3:10** Amu 20:1; 1Sam 25:28-31; 2Sam 24:2; 17:11; 1Fal 4:25
[b]**3:13** Mwa 43:5; 1Sam 18:20; Mwa 44:23-26
[c]**3:14** 1Sam 18:27
[d]**3:15** Kum 24:1-4; 1Sam 25:44
[e]**3:16** 2Sam 16:5; 17:18; 19:16
[f]**3:17** Amu 11:11
[g]**3:18** 1Sam 9:16; 2Sam 8:6; 1Sam 15:28
[h]**3:19** 1Nya 12:2, 16, 29; 1Sam 10:20-21
[i]**3:20** 1Nya 12:29
[j]**3:21** 2Sam 5:3; 1Fal 11:37; Kum 14:26; Za 20:4
[k]**3:25** Hes 27:17; Kum 28:6; 1Sam 29:6; Za 121:8; Isa 37:28
[l]**3:27** 2Sam 2:8; 4:1; 1Fal 2:5, 32; Kut 21:14; Amu 3:21; 2Sam 2:22-23; 20:9-10

vile kuzungumza naye faraghani. Ili kulipiza kisasi damu ya nduguye Asaheli, Yoabu akamchoma mkuki tumboni palepale, naye akafa.

28 [a]Baadaye, Daudi aliposikia kuhusu jambo hili, akasema, "Mimi na ufalme wangu kamwe hatuna hatia mbele za BWANA kuhusu damu ya Abneri mwana wa Neri. 29 [b]Damu yake na iwe juu ya kichwa cha Yoabu na juu ya nyumba yote ya baba yake! Kamwe asikosekane yeyote katika nyumba ya Yoabu mwenye kidonda chenye usaha, au ukoma au mwenye kuegemea fimbo au aangukaye kwa upanga au kupungukiwa na chakula."

30 [c](Yoabu na Abishai ndugu yake walimuua Abneri kwa sababu alikuwa amemuua Asaheli ndugu yao katika vita huko Gibeoni.)

31 [d]Kisha Daudi akamwambia Yoabu na watu wote aliokuwa pamoja nao, "Rarueni nguo zenu na mvae nguo za gunia na mtembee mkiomboleza mbele ya Abneri." Mfalme Daudi mwenyewe akatembea nyuma ya jeneza. 32 [e]Wakamzika Abneri huko Hebroni, naye mfalme akalia kwa sauti kwenye kaburi la Abneri. Pia watu wote wakalia.

33 [f]Mfalme akaimba ombolezo hili kwa ajili ya Abneri:

"Je, ilipasa Abneri afe kama afavyo
mpumbavu?
34 [g]Mikono yako haikufungwa,
miguu yako haikufungwa pingu.
Ulianguka kama yeye aangukaye
mbele ya watu waovu."

Nao watu wote wakamlilia tena.

35 [h]Kisha watu wote wakaja kumsihi Daudi ale chochote kulipokuwa kungali bado mchana; lakini Daudi akaapa, akisema, "Mungu na anishughulikie, tena kwa ukali, kama nikionja mkate au kitu kingine chochote kabla ya jua kutua!"

36 Watu wote wakaona hilo nao ikawapendeza; naam, kila kitu mfalme alichofanya kiliwapendeza. 37 Kwa hiyo siku ile watu wote na Israeli yote wakajua kwamba mfalme hakushiriki katika mauaji ya Abneri mwana wa Neri.

38 [i]Kisha mfalme akawaambia watu wake, "Je, hamfahamu kwamba mkuu na mtu mashuhuri ameanguka katika Israeli leo? 39 [j]Nami leo ingawa ni mfalme mpakwa mafuta, mimi ni dhaifu, nao hawa wana wa Seruya wananizidi nguvu. BWANA na amlipize mtenda maovu sawasawa na matendo yake maovu!"

*Ish-Boshethi Auawa*

4 [k]Ish-Boshethi mwana wa Sauli aliposikia kwamba Abneri amekufa huko Hebroni, akakosa ujasiri, nayo Israeli yote wakatiwa hofu kuu. 2 [l]Basi mwana wa Sauli alikuwa na watu wawili waliokuwa viongozi wa vikundi vya uvamizi. Mmoja aliitwa Baana na mwingine Rekabu, waliokuwa wana wa Rimoni, Mbeerothi, kutoka kabila la Benyamini. Beerothi alihesabiwa kuwa sehemu ya Benyamini, 3 [m]kwa sababu watu wa Beerothi walikimbilia huko Gitaimu na wameishi huko kama wageni mpaka siku hii ya leo.

4 [n](Yonathani mwana wa Sauli alikuwa na mwana aliyekuwa mlemavu miguu yote miwili. Alikuwa na miaka mitano wakati habari kuhusu Sauli na Yonathani

---

[a]**3:28** Kum 21:9
[b]**3:29** Law 20:9; 1Fal 2:31-33; Law 15:2; Amu 9:54-57; Za 7:11-16; Mit 2:22; 5:22
[c]**3:30** 2Sam 2:23
[d]**3:31** Za 30:11; 35:13; 69:11; Isa 20:2; Mwa 37:34; Yos 6:7; Amu 11:35; 2Fal 19:1; Ay 16:15; Yoe 1:8
[e]**3:32** Hes 14:1; Mit 24:17; 1Sam 31:4; 2Sam 18:33
[f]**3:33** Mwa 50:10; 2Sam 1:19; 13:13; Mhu 2:15-16
[g]**3:34** Ay 36:8; Za 2:3; 149:8; Isa 45:14; Nah 3:10
[h]**3:35** Rut 1:17; 1Sam 31:13; 2Sam 12:17; Yer 16:7; 1Sam 3:17
[i]**3:38** 2Sam 1:19
[j]**3:39** 2Sam 2:18; 16:9; 18:11; Amu 18:26; 1Fal 2:32; Za 41:10; 101:8; 2Sam 19:7, 13; Za 28:4; 62:12; 2Tim 4:14
[k]**4:1** 2Sam 3:27; Ezr 4:4
[l]**4:2** Yos 9:17; 18:25
[m]**4:3** Neh 11:33
[n]**4:4** 1Sam 18:1; 31:9; Law 21:18; 2Sam 9:8-12; 16:1-4; 19:24; 21:7-8; 1Nya 8:34; 9:40

zilipofika kutoka Yezreeli. Yaya wake
akambeba ili kukimbia, lakini yaya
alipokuwa anaharakisha kuondoka, mtoto
alianguka akawa kiwete. Jina lake aliitwa
Mefiboshethi.)
5 [a]Basi Rekabu na Baana, wana wa
Rimoni Mbeerothi wakaenda nyumbani
kwa Ish-Boshethi, nao walifika huko wakati
alipokuwa kwenye mapumziko yake ya
mchana. 6 [b]Wakaingia kwenye chumba cha
ndani kana kwamba wanachukua ngano,
wakamchoma Ish-Boshethi mkuki wa
tumboni. Ndipo Rekabu na Baana nduguye
wakatoroka.
7 [c]Walikuwa wameingia ndani ya nyumba
wakati alipokuwa amelala kitandani
chumbani kwake. Baada ya kumchoma
mkuki na kumuua, walikata kichwa chake.
Wakiwa wamekichukua, walitembea usiku
kucha kwa njia ya Araba. 8 [d]Wakamletea
Daudi kichwa cha Ish-Boshethi huko
Hebroni, wakamwambia mfalme, "Hiki
hapa kichwa cha Ish-Boshethi mwana wa
Sauli, adui yako, aliyejaribu kuondoa uhai
wako. Siku hii ya leo BWANA amemlipia
kisasi mfalme bwana wangu dhidi ya Sauli
na mzao wake."
9 [e]Daudi akawajibu Rekabu na Baana
nduguye, wana wa Rimoni, Mbeerothi,
akasema, "Hakika kama BWANA aishivyo,
ambaye ameniokoa kutoka taabu zote,
10 [f]yule mtu aliponiambia, 'Sauli amekufa,'
akadhani ananiletea habari njema,
nilimkamata, nikamuua huko Siklagi. Hiyo
ndiyo zawadi niliyompa kwa ajili ya taarifa
yake! 11 [g]Je, ni mara ngapi zaidi wakati
watu waovu wamemuua mtu asiye na hatia
akiwa ndani ya nyumba yake mwenyewe
na kwenye kitanda chake mwenyewe? Je,
sasa nisidai damu yake mikononi mwenu
na kuwaondoa duniani?"
12 [h]Kwa hiyo Daudi akawaamuru watu
wake, wakawaua. Wakakata mikono yao
na miguu, na kutundika viwiliwili vyao
kando ya dimbwi huko Hebroni. Lakini
wakakichukua kichwa cha Ish-Boshethi
na kukizika katika kaburi la Abneri huko
Hebroni.

*Daudi Atawazwa Mfalme Juu Ya Israeli*

**(1 Nyakati 11:1-9; 14:1-7)**

5 [i]Makabila yote ya Israeli yakamjia
Daudi huko Hebroni na kumwambia,
"Sisi tu nyama yako na damu yako hasa.
2 [j]Zamani, wakati Sauli alikuwa mfalme
juu yetu, wewe ndiwe uliyeiongoza Israeli
vitani. Naye BWANA alikuambia, 'Wewe
utawachunga watu wangu Israeli, na
utakuwa mtawala wao.' "
3 [k]Wazee wote wa Israeli wakamwendea
Mfalme Daudi huko Hebroni, mfalme
akafanya mapatano nao huko Hebroni
mbele za BWANA, nao wakamtia Daudi
mafuta kuwa mfalme wa Israeli.
4 [l]Daudi alikuwa na miaka thelathini
alipoanza kutawala, naye akatawala Israeli
miaka arobaini. 5 [m]Huko Hebroni alitawala
Yuda kwa miaka saba na miezi sita, na
katika Yerusalemu alitawala Israeli yote
na Yuda kwa miaka thelathini na mitatu.

*Daudi Ateka Yerusalemu*

6 [n]Mfalme na watu wake wakaenda
Yerusalemu kuwashambulia Wayebusi
walioishi humo. Wayebusi wakamwambia
Daudi, "Wewe hutaingia humu, kwani hata
vipofu na viwete wanaweza kukufukuza."
Walidhani, "Daudi hawezi kuingia humu."

---

[a]**4:5** 2Sam 2:8; Rut 2:7
[b]**4:6** 2Sam 2:23; Amu 5:25; Za 147:14
[c]**4:7** Kum 3:17; 1Sam 17:54; 31:9; Mt 14:11
[d]**4:8** 2Sam 20:21; 2Fal 10:7; 1Sam 24:4; 25:29; Hes 31:3; 1Sam 23:15
[e]**4:9** Mwa 48:16; 1Fal 1:29; Za 31:7; 103:4; 106:10
[f]**4:10** 2Sam 1:2-16
[g]**4:11** Mwa 4:10; 9:5; Za 9:12; 72:14
[h]**4:12** 2Sam 1:15; 3:32
[i]**5:1** 2Sam 19:43; Mwa 29:14; 35:26; 1Nya 11:1; 12:23
[j]**5:2** 1Sam 8:5, 13, 16; 11:6; Mwa 48:15; 1Sam 16:1; 2Sam 7:7; Mt 2:6; Yn 12:16; 1Sam 12:12; 13:14; 6:21; 25:30; Za 78:71
[k]**5:3** 2Sam 3:21; Kum 17:15; 2Sam 2:4; 1Nya 11:3; 2Fal 11:17; Amu 11:11; 1Sam 23:18
[l]**5:4** Mwa 37:2; Lk 3:23; 1Fal 2:11; 1Nya 3:4; 26:31; 29:27
[m]**5:5** 2Sam 2:11; 1Fal 2:11; 1Nya 3:4
[n]**5:6** Amu 1:8; Yos 15:8; Amu 1:21; 19:11

7 [a]Hata hivyo, Daudi akaiteka ngome ya
Sayuni, Mji wa Daudi.
8 [b]Siku ile, Daudi akasema, "Yeyote
ambaye atawashinda Wayebusi, atatumia
huo mfereji kuwafikia hao 'viwete na
vipofu' ambao ni adui za Daudi." Ndiyo
sababu wanasema, " 'Vipofu na viwete'
hawataingia kwenye jumba la ufalme."
9 [c]Ndipo Daudi akafanya makao ndani ya
ngome na kuiita Mji wa Daudi. Akajenga
eneo linalozunguka kuanzia Milo[d] kuelekea
ndani. 10 [e]Daudi akazidi kuwa na nguvu
zaidi na zaidi, kwa sababu BWANA Mungu
Mwenye Nguvu Zote alikuwa pamoja naye.
11 [f]Basi Hiramu mfalme wa Tiro
akawatuma wajumbe kwa Daudi, wakiwa na
magogo ya mierezi, maseremala na waashi,
nao wakajenga jumba la kifalme kwa ajili
ya Daudi. 12 [g]Naye Daudi akafahamu kuwa
BWANA amemwimarisha kuwa mfalme juu
ya Israeli na ameinua ufalme wake kwa ajili
ya Israeli, watu wake.
13 [h]Baada ya Daudi kuondoka Hebroni,
akajitwalia masuria zaidi na wake huko
Yerusalemu, nao wana na binti wengi
walizaliwa kwake. 14 [i]Haya ndiyo majina ya
watoto waliozaliwa kwake huko: Shamua,
Shobabu, Nathani, Solomoni, 15 Ibihari,
Elishua, Nefegi, Yafia, 16 Elishama, Eliada
na Elifeleti.

*Daudi Awashinda Wafilisti*

**(1 Nyakati 14:8-17)**

17 [j]Wafilisti waliposikia kuwa Daudi
ametiwa mafuta kuwa mfalme wa Israeli,
wakapanda na jeshi lao lote kwenda
kumsaka, lakini Daudi akapata habari
hizo, naye akateremka kwenye ngome.
18 [k]Basi Wafilisti walikuwa wamekuja na
kusambaa kwenye Bonde la Warefai, 19 [l]kwa
hiyo Daudi akamuuliza BWANA, "Je, niende
kuwashambulia Wafilisti? Je, utawatia
mikononi mwangu?"
BWANA akamjibu, "Nenda, kwa maana
hakika nitawatia Wafilisti mikononi
mwako."
20 [m]Ndipo Daudi akaenda mpaka Baal-
Perasimu, na huko akawashinda Wafilisti.
Akasema, "Kama mafuriko yafurikavyo,
BWANA amewafurikia adui zangu mbele
yangu." Kwa hiyo mahali hapo pakaitwa
Baal-Perasimu.[n] 21 [o]Wafilisti wakaiacha
miungu yao huko, naye Daudi na watu
wake wakaichukua.
22 Wafilisti walikwea kwa mara nyingine
na kusambaa katika Bonde la Warefai.
23 Kwa hiyo Daudi akamuuliza BWANA, naye
akamjibu, "Usipande moja kwa moja, bali
wazungukie kwa nyuma na uwashambulie
mbele ya miti ya miforosadi. 24 [p]Mara
utakaposikia sauti ya kutembea kutoka
kwenye vilele vya miti ya miforosadi, nenda
haraka, kwa sababu hiyo itamaanisha kuwa
BWANA ametangulia mbele yako kupiga
jeshi la Wafilisti." 25 [q]Basi Daudi akafanya
kama BWANA alivyomwagiza, naye
akawaangusha Wafilisti njia yote kuanzia
Geba[r] hadi Gezeri.

---

[a] **5:7** Za 76:2; Yer 21:13; 2Sam 6:12; 1Fal 2:10; 8:1; Isa 29:1; Yer 25:29
[b] **5:8** Yos 15:8; 17:15; 18:16; 1Nya 11:6
[c] **5:9** 2Fal 7:6; 1Fal 9:15, 24; 2Nya 32:5
[d] 9 Milo maana yake Boma la Ngome.
[e] **5:10** 2Sam 3:1; Za 24:10; 2Fal 7:9
[f] **5:11** 1Fal 15:1, 18; 2Nya 2:3; 1Fal 5:2; 1Nya 14:1
[g] **5:12** Hes 24:7; 1Fal 10:9; 2Nya 2:11; Es 4:14; Isa 45:4
[h] **5:13** Kum 17:17; 1Nya 3:9; Mwa 25:5-6
[i] **5:14** 1Nya 3:5; Lk 3:31
[j] **5:17** 2Sam 23:14; 1Nya 11:16
[k] **5:18** Yos 15:8; 17:15; 18:16; Isa 17:5
[l] **5:19** Amu 18:5; 1Sam 23:2; Hes 27:21; Yos 9:14
[m] **5:20** Mwa 38:29; Isa 28:21
[n] 20 Maana yake Bwana Afurikae.
[o] **5:21** Kum 7:5; Isa 46:2
[p] **5:24** Kut 14:24; Amu 4:14; 2Fal 7:6
[q] **5:25** 2Sam 8:12; 21:15; Isa 28:21; Yos 10:33; 1Nya 14:16
[r] 25 Kwa Kiebrania mji huu uliitwa Gibeoni (ona 1Nya 14:16).

*Sanduku La Mungu Laletwa Yerusalemu*

**(1 Nyakati 13:1-14; 15:25–16:6, 43)**

6 [a]Tena Daudi akakusanya watu 30,000
wa Israeli waliochaguliwa. 2 [b]Yeye na
watu wake wote wakatoka Baala ya Yuda[c]
kulipandisha Sanduku la Mungu kutoka
huko, linaloitwa kwa Jina, naam, jina la
BWANA Mwenye Nguvu Zote, ambaye
anaketi katika kiti cha enzi kati ya makerubi
walioko juu ya hilo Sanduku. 3 [d]Wakaweka
hilo Sanduku la Mungu juu ya gari jipya la
kukokotwa na kulileta kutoka nyumba ya
Abinadabu, iliyokuwa juu ya kilima. Uza
na Ahio, wana wa Abinadabu, walikuwa
wakiongoza hilo gari jipya la kukokotwa
4 likiwa na Sanduku la Mungu juu yake,
naye Ahio alikuwa anatembea akiwa mbele
yake. 5 [e]Daudi na nyumba yote ya Israeli
walikuwa wanacheza mbele za BWANA kwa
nguvu zao zote, kwa nyimbo, vinubi, zeze,
matari, kayamba na matoazi.

6 [f]Walipofika kwenye uwanja wa kupuria
nafaka wa Nakoni, Uza akanyoosha mkono
na kulishika Sanduku la Mungu kwa sababu
maksai walijikwaa. 7 [g]Hasira ya BWANA
ikawaka dhidi ya Uza kwa sababu ya
kitendo chake cha kukosa heshima, kwa
hiyo Mungu akampiga akafia papo hapo
kando ya Sanduku la Mungu.

8 [h]Ndipo Daudi akakasirika kwa sababu
ghadhabu ya BWANA ilifurika dhidi ya
Uza, hivyo hadi leo mahali hapo panaitwa
Peres-Uza.

9 [i]Daudi akamwogopa BWANA siku ile,
akasema, "Ni jinsi gani Sanduku la BWANA
litakavyoweza kunijia?" 10 [j]Hakuwa radhi
kulichukua Sanduku la BWANA kwake katika
Mji wa Daudi. Badala yake akalipeleka
kwenye nyumba ya Obed-Edomu, Mgiti.
11 [k]Sanduku la BWANA likabaki katika
nyumba ya Obed-Edomu, Mgiti, kwa miezi
mitatu, naye BWANA akambariki pamoja na
nyumba yake yote.

12 [l]Kisha Mfalme Daudi akaambiwa,
"BWANA ameibariki nyumba ya Obed-
Edomu pamoja na kila alicho nacho, kwa
sababu ya Sanduku la Mungu." Basi Daudi
akateremka na kulipandisha Sanduku la
Mungu kutoka nyumba ya Obed-Edomu
hadi Mji wa Daudi kwa shangwe. 13 [m]Wale
waliokuwa wamebeba Sanduku la BWANA
walipokuwa wametembea hatua sita,
Daudi alitoa dhabihu fahali na ndama
aliyenoneshwa. 14 [n]Daudi, akiwa amevaa
kisibau cha kitani, alicheza mbele za BWANA
kwa nguvu zake zote, 15 [o]wakati yeye na
nyumba yote ya Israeli walipopandisha
Sanduku la BWANA kwa shangwe na sauti
za tarumbeta.

16 [p]Ikawa Sanduku la BWANA lilipokuwa
linaingia katika Mji wa Daudi, Mikali
binti Sauli akachungulia dirishani. Naye
alipomwona Mfalme Daudi akirukaruka
na kucheza mbele za BWANA, akamdharau
moyoni mwake.

17 [q]Wakaleta Sanduku la BWANA na
kuliweka mahali pake ndani ya hema
ambalo Daudi alikuwa amelisimamisha
kwa ajili yake, naye Daudi akatoa sadaka za
kuteketezwa na sadaka za amani mbele za
BWANA. 18 [r]Baada ya kumaliza kutoa sadaka
za kuteketezwa na sadaka za amani, Daudi
akawabariki watu katika jina la BWANA

---

[a]**6:1** Za 80:1; 1Nya 13:5
[b]**6:2** Yos 15:9; 1Sam 4:4; 7:1; Law 24:16; Kum 28:10; Isa 63:10; Za 99:1; 132:14; Mwa 3:24; Kut 25:22
[c]2 Baala ya Yuda ni jina la Kiebrania; yaani Kiriath-Yearimu.
[d]**6:3** Hes 7:4-6; 1Sam 6:7; 2Sam 7:1
[e]**6:5** Kut 15:20; Ezr 3:10; Neh 12:27; Za 105:5
[f]**6:6** Hes 4:15, 19-20; 1Nya 13:9
[g]**6:7** 1Nya 15:13-15; Kut 19:23; 1Sam 5:6; 6:19; 25:32
[h]**6:8** Za 7:11; Mwa 38:29
[i]**6:9** 1Sam 6:20; Za 119:120; Hes 17:12-13; 1Sam 5:10-11; Lk 5:8
[j]**6:10** 1Nya 15:18; 26:4-5; 13:13
[k]**6:11** Mwa 30:27; 39:5; Mit 3:9-10; Isa 61:9
[l]**6:12** 1Fal 8:1; 1Nya 15:25
[m]**6:13** 1Fal 8:5, 62; Ezr 6:17; Hes 4:15; Yos 3:3; 1Nya 15:2, 15; 2Nya 5:6
[n]**6:14** Kut 19:6; 1Sam 2:18; Kut 15:20; Amu 11:34; 21:21; Za 30:11; 1Nya 15:27
[o]**6:15** Yos 6:5; Za 47:5; 98:6
[p]**6:16** 2Sam 5:7; 1Sam 18:27
[q]**6:17** 1Fal 8:6; 1Nya 15:1; 2Nya 1:4; Law 1:1-17; 1Fal 8:62-64; Za 132:8
[r]**6:18** 1Fal 8:22; Kut 39:43

Mwenye Nguvu Zote. 19 [a]Kisha akatoa
mkate, andazi la tende na andazi la zabibu
kavu kwa kila mtu katika mkutano wote
wa Waisraeli, wanaume kwa wanawake.
Nao watu wote wakaenda nyumbani kwao.
20 [b]Daudi aliporudi ili kuwabariki watu
wa nyumbani mwake, Mikali binti Sauli
akatoka nje kumlaki, akamwambia, "Tazama
jinsi mfalme wa Israeli alivyojibainisha
mwenyewe leo kwa kuvua mavazi yake
machoni pa vijakazi wa watumishi wake,
kama vile ambavyo mtu asiye na adabu
angelifanya!"
21 [c]Daudi akamwambia Mikali, "Nilifanya
hivyo mbele za BWANA ambaye alinichagua
mimi badala ya baba yako au mwingine
yeyote kutoka nyumba yake wakati
aliponiweka niwe mtawala juu ya Israeli,
watu wa BWANA. Kwa hiyo nitacheza mbele
za BWANA. 22 Nitakuwa asiye na heshima
zaidi kuliko sasa, nami nitajishusha machoni
pangu mwenyewe. Lakini kwa hawa vijakazi
uliosema habari zao nitaheshimiwa."
23 [d]Naye Mikali binti Sauli hakuwa na
watoto mpaka siku ya kufa kwake.

### *Ahadi Ya Mungu Kwa Daudi*

**(1 Nyakati 17:1-15)**

7 [e]Baada ya mfalme kuingia rasmi katika
jumba lake la kifalme, naye BWANA
akiwa amemstarehesha pande zote mbali
na adui zake, 2 [f]akamwambia nabii Nathani,
"Mimi hapa, ninaishi katika jumba la
kifalme la mierezi, wakati Sanduku la
Mungu limebaki katika hema."
3 [g]Nathani akamjibu mfalme, "Lolote
ulilo nalo moyoni, endelea ukalifanye, kwa
maana BWANA yu pamoja nawe."
4 Usiku ule neno la BWANA likamjia
Nathani, kusema:

5 [h]"Nenda ukamwambie mtumishi
wangu Daudi, 'Hili ndilo asemalo
BWANA: Je, ewe ndiwe wa kunijengea
mimi nyumba ili nikae ndani yake?
6 [i]Sijakaa ndani ya nyumba tangu
siku niliyowaleta Waisraeli kutoka
Misri hadi leo. Nimekuwa nikitembea
kutoka mahali pamoja hadi mahali
pengine ndani ya hema kama makao
yangu. 7 [j]Popote nilipotembea pamoja
na Waisraeli wote, je, nimewahi
kumwambia kiongozi wao yeyote
niliyemwamuru kuwachunga watu
wangu Israeli, "Kwa nini hujanijengea
nyumba ya mierezi?" '
8 [k]"Sasa basi, mwambie mtumishi
wangu Daudi, 'Hili ndilo asemalo
BWANA Mwenye Nguvu Zote: Nilikutoa
wewe kutoka machungani na kutoka
kuandama kundi la kondoo na mbuzi
ili kuwaongoza watu wangu Israeli.
9 [l]Nimekuwa pamoja nawe popote
ulipokwenda, nami nimekuondolea
mbali adui zako wote mbele yako. Basi
nitalifanya jina lako kuwa kuu kama
majina ya watu walio wakuu sana
duniani. 10 [m]Nami nitawapatia watu
wangu Israeli mahali niwapande humo
ili kwamba wawe na nyumbani kwao
wenyewe wasisumbuliwe tena. Watu
waovu hawatawaonea tena, kama

---

[a]**6:19** Hos 3:1; Kum 26:13; Neh 8:10
[b]**6:20** 1Sam 19:24; Mhu 7:16; Isa 59:15; Amu 9:4
[c]**6:21** 1Sam 13:14; 15:28; 2Sam 5:2; 7:8; 1Nya 5:2; 17:7; Mik 5:2
[d]**6:23** 1Sam 15:35; Isa 22:14
[e]**7:1** 1Nya 22:18; 17:1; 2Sam 6:3; Dan 4:29-30
[f]**7:2** 2Sam 12:1; 1Fal 1:8, 22; 1Nya 29:29; 2Nya 9:29; 2Sam 5:11; 1Fal 3:1; 7:1-7; 9:1; 2Nya 8:1; Yer 22:14; Hag 1:4; Kut 26:1; Za 132:3; Mdo 7:45-46; Kut 40:21
[g]**7:3** 1Sam 10:7; Za 132:1-5; 1Fal 8:17; 1Nya 22:7; 28:2
[h]**7:5** 1Fal 8:19; 1Nya 22:8; 1Fal 5:3-5; 1Nya 28:3
[i]**7:6** Mdo 7:45; Kut 40:18, 34; Yos 18:1; 1Fal 8:16
[j]**7:7** Kum 23:14; 2Sam 5:2; 1Fal 8:27; Isa 66:1; Law 26:11; Za 78:72; Eze 34:2, 15, 23; Mt 2:6; Mdo 20:28; 1Pet 5:2
[k]**7:8** 1Sam 16:11; 1Nya 21:17; Za 74:1; Amo 7:15; Isa 9:16; 16:1; 2Sam 6:21; Za 78:70-72; 2Kor 6:18
[l]**7:9** 1Sam 18:14; 2Sam 5:10; Za 18:37-42; Kut 11:3; Mwa 12:2; 1Nya 17:8; Lk 1:52
[m]**7:10** Kut 15:17; Isa 5:1-7; 2Fal 21:8; 2Nya 33:8; Za 89:22-23; 147:14; Isa 54:14; 60:18; Za 44:2; 80:8; Yer 24:6; Amo 9:15

walivyofanya mwanzoni, 11 [a]na kama
walivyofanya tangu mwanzo wakati
nilipowaweka viongozi juu ya watu
wangu Israeli. Pia nitawapa raha mbele
ya adui zenu wote.
"'Bwana akuambia kwamba
Bwana mwenyewe atakujengea
nyumba. 12 [b]Siku zako zitakapokwisha
nawe ulale pamoja na baba zako,
nitainua mzao wako aingie mahali
pako, ambaye atatoka viunoni
mwako, nami nitauimarisha ufalme
wake. 13 [c]Yeye ndiye atakayejenga
nyumba kwa ajili ya Jina langu,
nami nitaimarisha kiti cha enzi cha
ufalme wake milele. 14 [d]Nitakuwa
baba yake, naye atakuwa mwanangu.
Atakapokosea nitamwadhibu kwa
fimbo ya wanadamu, kwa adhabu
ya kupigwa na wanadamu. 15 [e]Lakini
upendo wangu kamwe hautaondolewa
kwake, kama nilivyouondoa kwa
Sauli, niliyemwondoa atoke mbele
yako. 16 Nyumba yako na ufalme
wako utadumu milele mbele zangu,
kiti chako cha enzi kitafanywa imara
milele.' "

17 Nathani akamwarifu Daudi maneno
yote ya maono haya.

*Maombi Ya Daudi*

**(1 Nyakati 17:16-27)**

18 [f]Ndipo Mfalme Daudi akaingia ndani,
akaketi mbele za Bwana, akasema:

"Ee Bwana Mwenyezi, mimi ni nani,
na jamaa yangu ni nini, hata umenileta
mpaka hapa nilipo? 19 [g]Naam, kana
kwamba hili halitoshi machoni pako,
Ee Bwana Mwenyezi, wewe umenena
pia kuhusu siku zijazo za nyumba ya
mtumishi wako. Je, hii ndiyo njia
yako ya kawaida ya kushughulika na
mwanadamu, Ee Bwana Mwenyezi?
20 [h]"Je, Daudi aweza kukuambia nini
zaidi? Kwa maana unamjua mtumishi
wako, Ee Bwana Mwenyezi. 21 [i]Kwa
ajili ya neno lako na kwa mapenzi
yako, umefanya jambo hili kubwa na
kulifanya lijulikane na lifahamike kwa
mtumishi wako.
22 [j]"Tazama jinsi ulivyo mkuu, Ee
Bwana Mwenyezi! Hakuna mwingine
kama wewe, wala hakuna Mungu ila
wewe, kama vile tulivyosikia kwa
masikio yetu wenyewe, 23 [k]Naye
ni nani aliye kama watu wako
Israeli, taifa pekee duniani ambalo
Mungu alitoka kwenda kulikomboa
kwa ajili yake mwenyewe, na
kujifanyia jina mwenyewe, kwa
kufanya maajabu makubwa na ya
kutisha kwa kuwafukuza mataifa na
miungu yao mbele ya watu wako,
ambao uliwakomboa kutoka Misri?
24 [l]Umeimarisha watu wako Israeli hasa
kama watu wako mwenyewe milele,
nawe, Ee Bwana, umekuwa Mungu
wao.

[a]**7:11** Amu 2:16; 1Sam 12:9-11; 1Fal 2:24; 1Sam 25:28; Za 89:35-37; Lk 1:32-33; Mdo 13:22-23; 2Tim 2:8; Kut 1:21; Isa 7:2
[b]**7:12** Mwa 15:15; 1Fal 2:1; Mdo 13:36; 1Fal 8:20; Za 132:11-12; Yer 30:21; 33:15; 2Nya 23:3
[c]**7:13** Kum 12:5; 1Fal 5:5; 6:12; 8:19, 29; Kum 16:11; 2Fal 21:4, 7; Mit 25:5; Dan 7:27; Mwa 9; 16; 2Sam 22:51; 1Fal 2:4, 45; 1Nya 22; 10; 28:6; 2Nya 6:16; 7:18; 13:5; 21:7; Za 89:3-4; Isa 9:7; 16:5; Yer 17:25; 33:17-21
[d]**7:14** Za 2:7; 89:26; Yer 3:19; Mt 3:17; Yn 1:49; 2Kor 6:18; Ebr 1:5; Ufu 21:7; Kum 8:5; 1Fal 11:34; 1Nya 22:10; Ebr 12:7; Za 89:30-33; Mit 13:24
[e]**7:15** 1Fal 2:4; 6:12; 8:25; 9:5; 11:13; 2Fal 19:34; 2Nya 6:16; 7:18; 21:7; Za 89:34; Yer 33; 17; 1Sam 13:13; 15:28; 16:14; 7:16; Za 89:36-37; Lk 1:33; Za 9:7; 93:2; 103:19
[f]**7:18** Kut 3:11; 1Sam 18:18
[g]**7:19** Isa 55:8-9
[h]**7:20** Isa 38:15; Yn 21:17; 1Sam 16:7; Mwa 18:19; Za 139:1
[i]**7:21** Efe 4:32
[j]**7:22** Za 48:1; 77; 13; 86:10; Yer 10:6; Kum 3:24; Kut 9:14; 8:10; 20:4; 10:2; Amu 6:13; 1Nya 16:25; 2Nya 2:5; Kum 4:35; Isa 45:5
[k]**7:23** Kum 4:32-38; 33:29; 1Sam 12:22; Hes 6:27; Kum 10:21; 7:7-8; 9:29; 15:15; Za 147:20; Neh 1:10
[l]**7:24** Kum 26:18; Kut 6:6-7; Za 48:14

25 [a]“Basi sasa, BWANA, ukaitimize
ahadi uliyosema kuhusu mtumishi
wako na nyumba yake milele. Fanya
kama ulivyoahidi, 26 [b]ili kwamba jina
lako litukuke milele. Ndipo watu
watasema, ‘BWANA Mwenye Nguvu
Zote ni Mungu juu ya Israeli!’ Nayo
nyumba ya mtumishi wako Daudi
itakuwa imara mbele zako.
27 “Ee BWANA Mwenye Nguvu Zote,
Mungu wa Israeli, umelifunua hili kwa
mtumishi wako, ukisema, ‘Nitakujengea
nyumba.’ Hivyo mtumishi wako
amepata ujasiri kukuletea dua hii.
28 [c]Ee BWANA Mwenyezi, wewe
ndiwe Mungu! Maneno yako ndiyo
kweli, nawe umemwahidi mtumishi
wako mambo haya mazuri. 29 [d]Sasa
naomba uwe radhi kuibariki nyumba
ya mtumishi wako, ili idumu mbele
zako milele, kwa maana wewe, Ee
BWANA Mwenyezi, umesema, na kwa
baraka zako nyumba ya mtumishi
wako itaendelea kubarikiwa milele.”

### *Ushindi Wa Daudi*

**(1 Nyakati 18:1-17)**

8 [e]Baada ya muda, Daudi akawashinda
Wafilisti na kuwatiisha, naye akautwaa
Metheg-Amma kutoka mikononi mwa
Wafilisti.
2 [f]Pia Daudi akawashinda Wamoabu.
Akawafanya walale chini kwa mstari
akawapima kwa urefu wa kamba. Kila
alipopima urefu wa hiyo kamba mara mbili
hilo kundi waliuawa na alipopima mara ya
tatu aliwaacha hai. Kwa hiyo Wamoabu
wakawa chini ya Daudi nao wakamletea
kodi.
3 [g]Zaidi ya hayo, Daudi akapigana na
Hadadezeri mwana wa Rehobu, mfalme wa
Soba, alipokwenda kurudisha tena utawala
wake kwenye eneo la Mto Frati. 4 [h]Daudi
akateka magari yake ya vita 1,000, askari
wapanda farasi 7,000 na askari 20,000
watembeao kwa miguu. Daudi akawakata
wale farasi wote wakokotao magari
mishipa ya miguu, isipokuwa farasi 100
hakuwakata.
5 [i]Waaramu wa Dameski walipokuja
kumsaidia Hadadezeri mfalme wa Soba,
Daudi akawashambulia na kuwaua 22,000
miongoni mwao. 6 [j]Daudi akaweka askari
walinzi katika ufalme wa Waaramu huko
Dameski, nao Waaramu wakawa watumwa
wake na kumlipa ushuru. BWANA akampa
Daudi ushindi kote alipokwenda.
7 [k]Daudi akazitwaa ngao za dhahabu
zilizokuwa za maafisa wa Hadadezeri na
kuzileta Yerusalemu. 8 [l]Kutoka miji ya Beta[m]
na Berothai, iliyokuwa miji ya Hadadezeri,
Mfalme Daudi akatwaa shaba nyingi sana.
9 [n]Tou, mfalme wa Hamathi, aliposikia
kwamba Daudi amelishinda jeshi lote
la Hadadezeri, 10 akamtuma mwanawe
Yoramu kwa Mfalme Daudi kumsalimu na
kumpongeza kwa ushindi wake katika vita
dhidi ya Hadadezeri, kwa kuwa Hadadezeri
alikuwa amepigana vita na Tou. Yoramu
akamletea Daudi vyombo vya fedha,
dhahabu na shaba.
11 [o]Mfalme Daudi akaviweka vifaa hivi
wakfu kwa BWANA, kama vile alivyokuwa
amefanya kwa fedha na dhahabu kutoka
kwa mataifa yote aliyokuwa ameyashinda:
12 [p]yaani Edomu, Moabu, Waamoni, Wafilisti

---

[a]**7:25** Hes 23:19; 2Nya 1:9
[b]**7:26** Kut 6:3; Neh 9:5; Za 72:19; 96:8; Mt 6:9; 1Sam 25:28
[c]**7:28** Kut 34:6; Yn 17:17
[d]**7:29** Hes 6:23-27
[e]**8:1** 2Sam 7:9; 21:15-22; 1Nya 18:1
[f]**8:2** Mwa 19:37; Hes 21:29; Amu 3:15; Isa 45:14; Hes 24:17; 1Sam 14:47; Za 50:8; 72:10
[g]**8:3** 2Sam 10:16; 1Fal 11:23; 1Sam 14:47; Mwa 2:14; 15:18
[h]**8:4** Mwa 49:6; Yos 11:9
[i]**8:5** Mwa 14:15; 2Sam 10:6; 1Fal 11:24; 2Fal 8:7; 14:28
[j]**8:6** 1Fal 20:34; 2Fal 10:19; 2Sam 3:18
[k]**8:7** 1Fal 10:16; 14:26; 2Fal 11:10
[l]**8:8** Eze 47:16
[m]8 Beta ulikuwa mji wa Aramu-Soba ambao uliitwa Teba kwa Kiaramu; pia uliitwa Tibhathi (1Nya 18:8).
[n]**8:9** 1Fal 8:65; 2Fal 14:28; 2Nya 8:4; Lk 14:31-32
[o]**8:11** 1Fal 7:51; 15:15; 1Nya 26:26; 2Nya 5:1; 1Nya 18:11; 22:14-16; Mik 4:13; Ufu 21:24
[p]**8:12** 2Sam 10:14; 5:25; Hes 24:20; 1Sam 27:8

na Waamaleki. Pia akaweka wakfu nyara
alizoteka kutoka kwa Hadadezeri mwana
wa Rehobu, mfalme wa Soba.
13 [a]Naye Daudi akapata sifa baada ya
kurudi kutoka kuwaua Waedomu 18,000
katika Bonde la Chumvi.
14 [b]Akaweka kambi za askari walinzi
katika Edomu yote, nao Waedomu wakakawa
chini ya Daudi. BWANA alimpatia Daudi
ushindi kila alipokwenda.

*Maafisa Wa Daudi*

15 [c]Daudi akatawala Israeli yote, akitenda
lililo haki na sawa kwa watu wake wote.
16 [d]Yoabu mwana wa Seruya alikuwa
jemadari wa jeshi; Yehoshafati mwana wa
Ahiludi alikuwa mweka kumbukumbu;
17 [e]Sadoki mwana wa Ahitubu na Ahimeleki
mwana wa Abiathari walikuwa makuhani;
Seraya alikuwa mwandishi; 18 [f]Benaya
mwana wa Yehoyada alikuwa msimamizi
wa Wakerethi na Wapelethi; nao wana wa
Daudi walikuwa washauri wa mfalme.

*Daudi Na Mefiboshethi*

9 [g]Daudi akauliza, "Je, hakuna mtu hata
mmoja wa nyumba ya Sauli aliyebaki
ambaye naweza kumtendea wema kwa ajili
ya Yonathani?"
2 [h]Basi palikuwepo mtumishi wa nyumba
ya Sauli aliyeitwa Siba. Wakamwita aje
mbele ya Daudi, naye mfalme akamwambia,
"Wewe ndiwe Siba?"
Akamjibu, "Naam, mimi ndiye mtumishi
wako."
3 [i]Mfalme akauliza, "Je, hakuna yeyote
ambaye amebaki wa nyumba ya Sauli
ninayeweza kumwonyesha wema wa
Mungu?"
Siba akamjibu mfalme, "Bado yupo
mwana wa Yonathani, yeye ni kiwete
miguu yote."
4 [j]Mfalme akauliza, "Yuko wapi?"
Siba akajibu, "Yuko nyumbani kwa
Makiri mwana wa Amieli huko Lo-Debari."
5 Basi Mfalme Daudi akamtaka aletwe
kutoka Lo-Debari, kutoka nyumbani kwa
Makiri mwana wa Amieli.
6 [k]Mefiboshethi mwana wa Yonathani,
mwana wa Sauli, alipofika kwa Daudi,
akainama kumpa mfalme heshima.
Daudi akamwita, "Mefiboshethi!"
Mefiboshethi akajibu, "Ndimi mtumishi
wako."
7 [l]Daudi akamwambia, "Usiogope, kwa
maana hakika nitakutendea wema kwa ajili
ya baba yako Yonathani. Nitakurudishia
ardhi yote iliyokuwa mali ya Sauli baba
yako, nawe daima utakula chakula mezani
pangu."
8 [m]Mefiboshethi akasujudu akasema,
"Mimi mtumishi wako ni nini hata uangalie
mbwa mfu kama mimi?"
9 [n]Ndipo mfalme akamwita Siba mtumishi
wa Sauli na kumwambia, "Nimempa mwana
wa bwana wako kila kitu kilichokuwa mali
ya Sauli na jamaa yake. 10 [o]Wewe, wanao
na watumishi wako mtamlimia mashamba
Mefiboshethi na kumletea mavuno, ili
kwamba mwana wa bwana wako apate
mahitaji yake. Naye Mefiboshethi mwana

---

[a]**8:13** 2Sam 7:9; 2Fal 14:7; 1Nya 18:12; Za 60
[b]**8:14** Hes 24:17-18; Za 108:9; Isa 34:5; 63:1; Yer 49:7; Eze 25:12; Mwa 27:29, 37-40; Za 144:10; 2Sam 22:44; Za 18:43
[c]**8:15** Mwa 18:19; 1Fal 11:18; 14:8; 15:11; 22:43; 2Fal 12:2; Ay 29:14; Za 5:12; 119:121; Ebr 11:33
[d]**8:16** 2Sam 2:13; 20:24; 1Fal 4:3; Isa 36:3, 22; 2Sam 19:13
[e]**8:17** 1Sam 2:35; 15:24, 29; 2Sam 20:25; 1Fal 1:8; 4:4; 1Nya 6:8, 53; 16:39; 24:3; 27:17; 2Nya 13:10; Eze 40:46; 43:19; 44:15; 48:11; Mk 2:26; 1Fal 4:3; 2Fal 12:10; 19:2; 22:3; Isa 36:3; Yer 36:12
[f]**8:18** 2Sam 20:23; 23:20; 1Fal 1:8; 2:25, 35, 46; 4:4; 1Sam 30:14; 1Nya 18:17
[g]**9:1** 1Sam 20:14-17, 42; 23:18; 18:3; Mit 27:10
[h]**9:2** 2Sam 16:1-4; 19:17, 26-29

---

[i]**9:3** 1Nya 8:34; Law 21:18; 1Sam 20:14; 2Sam 4:4; Kum 19:15; Mt 5:44; Lk 6:36; Tit 3:3-4
[j]**9:4** 2Sam 17:27-29
[k]**9:6** Mwa 37:7; 2Sam 16:4
[l]**9:7** 1Sam 20:14-15; 2Sam 19:28; 21:7; 1Fal 2:7; 2Fal 25:29; Yer 52:33; Mwa 43:18; 50:21; 1Sam 12:19-24; Yer 52:33
[m]**9:8** 2Sam 4:4; 3:8; 1Sam 24:14; 2Sam 16:9
[n]**9:9** Isa 32:8
[o]**9:10** 2Sam 16:3; 19:28

wa bwana wako atakula chakula mezani
pangu daima.” (Siba alikuwa na wana kumi
na watano, na watumishi ishirini.)
11 [a]Ndipo Siba akamwambia mfalme,
“Mtumishi wako atafanya chochote bwana
wangu mfalme atakachoagiza mtumishi
wake kufanya.” Basi Mefiboshethi akala
chakula mezani pa Daudi kama mmoja wa
wana wa mfalme.
12 [b]Mefiboshethi alikuwa na mwanawe
mdogo aliyeitwa Mika, nao watu wote wa
nyumba ya Siba walikuwa watumishi wa
Mefiboshethi. 13 [c]Naye Mefiboshethi akaishi
huko Yerusalemu, kwa sababu daima
alikula mezani pa mfalme, naye alikuwa
kiwete miguu yote.

*Daudi Awashinda Waamoni*

**(1 Nyakati 19:1-19)**

10 [d]Baada ya muda, mfalme wa
Waamoni akafa, naye Hanuni
mwanawe akaingia mahali pake. 2 [e]Daudi
akawaza, “Nitamtendea wema Hanuni
mwana wa Nahashi, kama vile baba yake
alivyonitendea mimi wema.” Hivyo Daudi
akatuma wajumbe kuonyesha wema wake
kwa Hanuni kuhusu baba yake.
Watu wa Daudi walipofika katika nchi
ya Waamoni, 3 [f]wakuu wa Waamoni
wakamwambia Hanuni bwana wao,
“unadhani Daudi anamheshimu baba
yako kwa kukutumia watu ili kuonyesha
masikitiko? Je, Daudi hakuwatuma watu
hawa kuchunguza na kuupeleleza mji ili
kuupindua?” 4 [g]Basi Hanuni akawakamata
watu wa Daudi, akawanyoa kila mmoja
ndevu zake nusu, akakata mavazi yao
nyuma katikati kwenye matako, akawaacha
waende zao.
5 Daudi alipoambiwa jambo hili, akatuma
wajumbe ili kwenda kuwalaki, kwa maana
walikuwa wamevunjiwa heshima sana.
Mfalme akasema, “Kaeni huko Yeriko
mpaka ndevu zenu ziote ndipo mje.”
6 [h]Waamoni walipotambua kuwa
wamekuwa machukizo kwa Daudi, wakaajiri
askari wa miguu 20,000 Waaramu kutoka
Beth-Rehobu na Soba, pia mfalme wa
Maaka pamoja na watu 1,000, na vilevile
watu 12,000 kutoka Tobu.
7 [i]Daudi aliposikia jambo hili, akamtuma
Yoabu na jeshi lote la wapiganaji.
8 Waamoni wakatoka wakajipanga wakiwa
tayari kwa vita langoni la mji wao, wakati
Waaramu wa Soba, wa Rehobu, watu wa
Tobu na Maaka walikuwa peke yao kwenye
eneo la wazi.
9 Yoabu akaona kuwa mbele yake na
nyuma yake kumepangwa vita; kwa hiyo
akachagua baadhi ya vikosi vilivyo bora
sana katika Israeli akavipanga dhidi ya
Waaramu. 10 [j]Akawaweka waliobaki
chini ya uongozi wa Abishai nduguye na
kuwapanga dhidi ya Waamoni. 11 Yoabu
akasema, “Kama Waaramu watanizidi
nguvu, basi itawabidi mje kunisaidia.
Lakini kama Waamoni watawazidi nguvu,
basi nitakuja kuwasaidia. 12 [k]Uwe hodari na
tupigane kwa ujasiri kwa ajili ya watu wetu
na miji ya Mungu wetu. BWANA atafanya
lile lililo jema machoni pake.”
13 Basi Yoabu na vikosi vyake wakasonga
mbele kupigana na Waaramu, nao Waaramu
wakakimbia mbele yake. 14 [l]Waamoni
walipoona Waaramu wanakimbia,
nao wakakimbia mbele ya Abishai na
kuingia ndani ya mji. Basi Yoabu akarudi
kutoka kupigana na Waamoni na kufika
Yerusalemu.

[a]**9:11** Ay 36:7; Za 113:8; 1Sam 16:1-4; Mit 12:17
[b]**9:12** 2Sam 4:4; 1Nya 8:34
[c]**9:13** 2Sam 19:33-36; 2Fal 25:29; Yer 52:33-34
[d]**10:1** 1Sam 11:1; 2Sam 17:27; 1Nya 19:1
[e]**10:2** 1Sam 11:1
[f]**10:3** Hes 21:32
[g]**10:4** Law 19:27; Isa 7:20; 15:2; 50:6; 52:14; Yer 48:37; Eze 5:1; Isa 20:4; 3:17; Yer 13:22; Eze 16:37; Mik 1:11; Nah 3:5
[h]**10:6** Mwa 34:30; 2Sam 8; 5; Hes 13:21; 1Sam 14:47; Kum 3:14; Amu 11:3-5; 18:28; Kut 5:21; 1Sam 13:4
[i]**10:7** 2Sam 2:18; 23:8
[j]**10:10** 1Sam 26:6
[k]**10:12** Kum 1:21; 31:6; Efe 6:10; Amu 10:15; Neh 4:14; 1Kor 16:3; 1Sam 3:18; 2Nya 19:11; 1Sam 4:9; 2Sam 15:26; 22:31-32; Za 20:7; 37:4-5; Mit 29:25
[l]**10:14** 2Sam 8:12

15 Baada ya Waaramu kuona
wameshindwa na Israeli, wakajikusanya
tena. 16 Hadadezeri akaagiza Waaramu
walioletwa kutoka ng'ambo ya Mto
Frati, wakaenda Helamu pamoja na
Shobaki jemadari wa jeshi la Hadadezeri
akiwaongoza.
17 Daudi alipoambiwa haya,
akawakusanya Israeli wote, wakavuka
Mto Yordani, wakaenda Helamu. Waaramu
wakapanga vikosi vyao vya askari
kukabiliana na kupigana dhidi ya Daudi.
18 Lakini Waaramu wakakimbia mbele ya
Israeli, naye Daudi akawaua waendesha
magari mia saba na askari wao wa miguu
40,000. Vilevile alimpiga Shobaki jemadari
wa jeshi lao, naye akafa huko. 19 [a]Wafalme
wote waliokuwa wanamtumikia Hadadezeri
walipoona kuwa wameshindwa na Israeli,
wakafanya amani na Waisraeli na wakawa
chini yao.

Hivyo Waaramu wakaogopa kuwasaidia
Waamoni tena.

### *Daudi Na Bathsheba*

11 [b]Katika mwanzo wa mwaka mpya,
wakati wafalme watokapo kwenda
vitani, Daudi akamtuma Yoabu pamoja na
watu wa mfalme na jeshi lote la Israeli.
Wakawaangamiza Waamoni na kuuzunguka
kwa jeshi mji wa Raba. Lakini Daudi
akabaki Yerusalemu.
2 [c]Ikawa siku moja wakati wa jioni
Daudi aliinuka kitandani mwake na
kutembeatembea juu ya paa la jumba
lake la kifalme. Kutokea kule kwenye paa,
akamwona mwanamke akioga. Mwanamke
huyo alikuwa mzuri sana wa sura, 3 [d]naye
Daudi akatuma mtu mmoja kuuliza
habari za huyo mwanamke. Huyo mtu
akamwambia Daudi, "Je, huyu si Bathsheba
binti Eliamu, naye ni mke wa Uria, Mhiti?"
4 [e]Ndipo Daudi akatuma wajumbe kumleta.
Huyo mwanamke akaja kwa Daudi, Daudi
akakutana naye kimwili. (Huyo mwanamke
ndipo tu alikuwa amejitakasa kutoka siku
zake za hedhi.) Kisha akarudi nyumbani
kwake. 5 [f]Huyo mwanamke akapata mimba
akampelekea Daudi ujumbe, kusema, "Mimi
ni mjamzito."
6 [g]Ndipo Daudi akapeleka ujumbe kwa
Yoabu, "Unipelekee Uria, Mhiti." Naye
Yoabu akamtuma Uria kwa Daudi. 7 Uria
alipofika, Daudi akamuuliza habari za
Yoabu, hali za askari na vita kwamba
inaendeleaje. 8 [h]Kisha Daudi akamwambia
Uria, "Teremka nyumbani kwako ukanawe
miguu yako." Basi Uria akaondoka kutoka
kwenye jumba la kifalme, tena zawadi
zikamfuata kutoka kwa mfalme. 9 [i]Lakini
Uria akalala kwenye ingilio la jumba la
kifalme pamoja na watumishi wote wa
bwana wake, na hakuteremka kwenda
nyumbani kwake.
10 Daudi alipoambiwa kwamba, "Uria
hakwenda nyumbani," Daudi akamuuliza,
"Je, si ndiyo tu umefika kutoka safari ya
mbali? Kwa nini hukwenda nyumbani?"
11 [j]Uria akamwambia Daudi, "Sanduku la
Mungu, na Israeli na Yuda wanakaa kwenye
mahema, naye bwana wangu Yoabu na watu
wa bwana wangu wamepiga kambi mahali
pa wazi. Ningewezaje kwenda nyumbani
kwangu ili nile, ninywe na kukutana na mke
wangu? Hakika kama uishivyo sitafanya
jambo la namna hiyo!"
12 [k]Ndipo Daudi akamwambia, "Kaa hapa
siku moja zaidi, nami kesho nitakutuma
urudi." Kwa hiyo Uria akakaa Yerusalemu

[a]**10:19** 2Sam 8:6; 1Fal 11:25; 22:31; 2Fal 5:1; Mwa 14:4
[b]**11:1** 1Fal 20:22; 2Sam 2:18; 1Nya 20:1; Kum 3:11
[c]**11:2** Kum 22:8; Yos 2:8; Mt 5:28; Mwa 34:2; Ay 31:1; Za 119:37
[d]**11:3** 1Nya 3:5; 2Sam 23:34-39
[e]**11:4** Law 20:10; Za 51; Yak 1:14-15; Kum 22:22; Law 15:25-30; 18:19; Kut 20:17; Ebr 13:4
[f]**11:5** Law 20:10
[g]**11:6** 1Nya 11:41
[h]**11:8** Mwa 18:4; 43:24; Lk 7:44; Za 44:21; Mwa 19:2
[i]**11:9** Ay 5:12-14
[j]**11:11** 2Sam 7:2; 1Sam 21:5; 4:4; 2Sam 20:6; Mt 10:25; 2Tim 2:3
[k]**11:12** Ay 20:12-14; Yer 2:22-23

siku ile na siku iliyofuata. 13 [a]Kwa ukaribisho
wa Daudi, Uria akala na kunywa pamoja
naye, Daudi akamlevya. Lakini jioni Uria
alitoka kwenda kulala juu ya mkeka wake
miongoni mwa watumishi wa bwana wake,
hakwenda nyumbani.
14 [b]Asubuhi yake Daudi akamwandikia
Yoabu barua, akamtuma Uria kuipeleka.
15 [c]Ndani ya barua aliandika, “Mweke Uria
mstari wa mbele mahali ambapo mapigano
ni makali sana. Kisha wewe uondoke ili Uria
aangushwe chini na kuuawa.”
16 Hivyo Yoabu alipokuwa ameuzingira
mji kwa jeshi, akamweka Uria mahali
ambapo alijua kuwa ulinzi wa adui
ulikuwa imara sana. 17 Wakati watu wa
mjini walipotoka kwenda kupigana dhidi
ya Yoabu, baadhi ya watu katika jeshi la
Daudi wakauawa, zaidi ya hayo, Uria,
Mhiti, akafa.
18 Yoabu akampelekea Daudi maelezo
yote ya vita. 19 Akamwagiza mjumbe hivi,
“Utakapokuwa umemaliza kumpa mfalme
maelezo ya vita, 20 hasira ya mfalme yaweza
kuwaka, naye aweza kukuuliza, ‘Kwa nini
mlisogea karibu hivyo na mji kupigana?
Hamkujua kuwa wangeweza kuwapiga
mishale kutoka ukutani? 21 [d]Ni nani
aliyemuua Abimeleki mwana wa Yerub-
Besheth? Je, mwanamke hakutupa juu yake
jiwe la juu la kusagia kutoka ukutani, kwa
hiyo akafa huko Thebesi? Kwa nini mlisogea
hivyo karibu ya ukuta?’ Ikiwa atakuuliza
hivi, ndipo umwambie, ‘Pia mtumishi wako
Uria, Mhiti, amekufa.’ ”
22 Mjumbe akaondoka. Alipowasili
akamwambia Daudi kila kitu alichokuwa
ametumwa na Yoabu kusema. 23 Mjumbe
akamwambia Daudi, “Watu walituzidi
nguvu wakatoka nje ya mji dhidi yetu
kwenye eneo la wazi, lakini tuliwarudisha
nyuma mpaka kwenye ingilio la mji.
24 Ndipo wapiga upinde walitupa mishale
kwa watumishi wako kutoka ukutani, na
baadhi ya watu wa mfalme wakafa. Zaidi
ya hayo, Uria, Mhiti, mtumishi wako
amekufa.”
25 Daudi akamwambia mjumbe,
“Ukamwambie Yoabu hivi, ‘Jambo hili
lisikutie wasiwasi, upanga hula huyu sawa
na ulavyo mwingine. Zidisha mashambulizi
dhidi ya mji na uangamize.’ Mwambie
Yoabu hivi ili kumtia moyo.”
26 Mke wa Uria aliposikia kwamba
mumewe amekufa, akamwombolezea.
27 [e]Baada ya muda wa maombolezo kwisha,
Daudi akamtaka aletwe nyumbani kwake,
naye akawa mkewe, na akamzalia mwana.
Lakini jambo alilokuwa amefanya Daudi
lilimchukiza Bwana.

*Nathani Amkemea Daudi*

12 [f]Bwana akamtuma Nathani kwa
Daudi. Alipofika kwake akamwambia,
“Katika mji mmoja kulikuwepo na watu
wawili, mmoja alikuwa tajiri na mwingine
alikuwa maskini. 2 Yule mtu tajiri alikuwa
na idadi kubwa sana ya kondoo na
ng’ombe, 3 lakini yule maskini hakuwa na
chochote ila kondoo jike mdogo aliyekuwa
amemnunua. Akamtunza kondoo huyo,
akakulia kwake pamoja na watoto wake.
Kondoo huyo alishiriki chakula cha bwana
wake na kunywea kikombe chake hata pia
huyo kondoo alilala mikononi mwa bwana
wake. Kwake alikuwa kama binti yake.
4 “Siku moja yule tajiri akafikiwa
na mgeni, lakini huyo tajiri akaacha
kuchukua mmoja wa kondoo au ng’ombe
wake mwenyewe amwandalie mgeni.
Badala yake akachukua yule kondoo jike
mdogo aliyekuwa mali ya yule maskini na
kumwandalia yule mgeni wake.”
5 [g]Daudi akawakwa na hasira dhidi ya
mtu huyo tajiri na kumwambia Nathani,
“Hakika kama Bwana aishivyo, mtu huyo

[a]**11:13** Mwa 9:21-22; 19:33-35; Kut 32:21; 1Fal 20:16-21; Mit 20:1; 23:29-35; Hos 4:11; Gal 5:21
[b]**11:14** 1Fal 21:8; Za 19:13; 62:9; Mhu 8:11; Yer 9:1-4; Mik 7:3-5
[c]**11:15** 2Sam 12:9; 12:12
[d]**11:21** Amu 8:31; 9:50-54; 2Sam 20:21; Ay 31:3
[e]**11:27** Kum 34:8; 2Sam 12:9; Za 51:4-5; Ay 10:14; 11:11; Za 45:7; Mit 15:9; Hab 1:13
[f]**12:1** 1Fal 20:35-41; Za 51; 2Sam 14:4; 7:2; Mt 21:33, 45; Lk 15:11
[g]**12:5** 1Fal 20:40; Mwa 34:7; Rum 2:1; 1Sam 14:39

aliyefanya hivyo anastahili kufa! 6 [a]Lazima
alipe mara nne zaidi, kwa ajili ya kondoo
huyo, kwa sababu amefanya jambo kama
hilo na hakuwa na huruma.”
7 [b]Ndipo Nathani akamwambia Daudi,
“Wewe ndiwe huyo mtu! Hivi ndivyo
asemavyo BWANA, Mungu wa Israeli:
‘Nilikupaka mafuta uwe mfalme juu ya
Israeli, nilikuokoa kutokana na mkono
wa Sauli. 8 [c]Nilikupa nyumba ya bwana
wako na wake za bwana wako mikononi
mwako. Nikakupa nyumba ya Israeli na
Yuda. Kama haya yote yalikuwa madogo
sana, ningekupa hata zaidi. 9 [d]Kwa nini
ulilidharau neno la BWANA kwa kufanya
lililo ovu machoni pake? Ulimuua Uria,
Mhiti kwa upanga na kumchukua mke
wake awe mkeo. Ulimuua kwa upanga
wa Waamoni. 10 [e]Basi kwa hiyo, upanga
hautaondoka nyumbani mwako kamwe kwa
sababu ulinidharau mimi na kumchukua
mke wa Uria, Mhiti kuwa mkeo.’
11 [f]“Hili ndilo asemalo BWANA: ‘Kutoka
kwa nyumba yako mwenyewe nitaleta
maafa juu yako. Mbele ya macho yako
mwenyewe nitatwaa wake zako na kumpa
yeye aliye wa karibu nawe, naye atakutana
kimwili na wake zako mchana mwangavu.
12 [g]Ulifanya kwa siri, lakini nitalifanya
jambo hili wakati wa mchana mwangavu
mbele ya Israeli yote.’ ”
13 [h]Ndipo Daudi akamjibu Nathani,
“Nimefanya dhambi dhidi ya BWANA.”
Nathani akamjibu, “BWANA
amekuondolea dhambi yako. Hutakufa.
14 [i]Lakini kwa sababu kwa kufanya hili
umefanya adui za BWANA kuonyesha
dharau kabisa, mwana atakayezaliwa
kwako atakufa.”
15 [jk]Baada ya Nathani kurudi nyumbani
kwake, BWANA akampiga yule mtoto
ambaye mke wa Uria alikuwa amemzalia
Daudi, akaugua. 16 [l]Daudi akamwomba
Mungu kwa ajili ya mtoto. Akafunga na
akaingia ndani ya nyumba yake akawa siku
zote analala sakafuni usiku kucha. 17 [m]Wazee
wa nyumbani mwake wakamwendea
wakasimama karibu naye ili kumwamsha
kutoka pale sakafuni, lakini akakataa, wala
hakula chochote pamoja nao.
18 Kunako siku ya saba yule mtoto
akafa. Watumishi wa Daudi wakaogopa
kumwambia kuwa mtoto amekufa, kwa
maana walifikiri, “Wakati mtoto alipokuwa
angali hai, tulizungumza na Daudi lakini
hakutusikiliza. Tutawezaje kumwambia
kwamba mtoto amekufa? Anaweza kufanya
kitu cha kujidhuru.”
19 Daudi akaona kuwa watumishi
wake wananong’onezana wenyewe, naye
akatambua kuwa mtoto alikuwa amekufa.
Akauliza “Je, ni kwamba huyo mtoto
amekufa?”
Wakamjibu, “Ndiyo, mtoto amekufa.”
20 [n]Basi Daudi akainuka kutoka pale
sakafuni. Baada ya kuoga, akajipaka mafuta
na kubadilisha nguo zake kisha akaenda
ndani ya nyumba ya BWANA, akaabudu.
Baada ya hapo akaenda nyumbani kwake
kwa kutaka kwake, wakamwandalia
chakula, naye akala.
21 [o]Watumishi wake wakamuuliza, “Kwa
nini unafanya hivi? Mtoto alipokuwa angali

[a]**12:6** Kut 22:1; Lk 19:8
[b]**12:7** 1Sam 14:13; Dan 4:22; 1Sam 2:35; 1Fal 20:42; 1Sam 16:13; 2Sam 7:8
[c]**12:8** 2Sam 9:7
[d]**12:9** Hes 15:31; 1Sam 13:14; 2Sam 11:15; 1Fal 15:5; Za 26:9; 51:14; Mwa 9:5-6; 1Sam 15:19; Law 26:15-16; Mit 13:13; Isa 5:24
[e]**12:10** 2Sam 13:28; 18:14-15; 1Fal 2:25; 2Sam 11:15
[f]**12:11** 2Sam 16:11, 21-22; Kum 28:30; 17:17
[g]**12:12** 2Sam 11:14-15; 16:22
[h]**12:13** Mwa 13:13; 20:6; Hes 22:34; Za 32:1-5; 51:1-9; 103:12; Isa 43:25; 44:22; Zek 3:4-9; Mit 28:13; Yer 2:35; Mik 7:18-19; Law 20:10; 24:17
[i]**12:14** Isa 52:5; Rum 2:24; Eze 36:20
[j]**12:15** 1Sam 25:38; Mwa 4:7; Amo 3:2
[k]**12:15** 2Sam 5:25
[l]**12:16** 2Sam 13:31; Za 5:7; 95:6; Isa 26:16; Yer 18:8; 50:4; Amu 20:26; Yoe 1:14
[m]**12:17** Mwa 37:35; 1Sam 1:7; 2Sam 3:35; Dan 6:18
[n]**12:20** Mt 6:17; Mwa 41:14; Ay 1:20; Rut 3:3; Za 95:6-8; 103:8-17; Mit 3:7; 16:6; Mao 3:40-41
[o]**12:21** Amu 20:26

hai, ulifunga na kulia; lakini sasa mtoto
amekufa, umeinuka na kula.”
22 [a]Akajibu, “Wakati mtoto alipokuwa
bado yungali hai, nilifunga na kulia.
Nilifikiri, ‘Nani ajuaye? BWANA aweza
kunirehemu ili kumwacha mtoto aishi.’
23 [b]Lakini sasa kwa kuwa amekufa, kwa
nini nifunge? Je, naweza kumrudisha
tena? Mimi nitakwenda kwake, lakini yeye
hatanirudia mimi.”
24 [c]Ndipo Daudi akamfariji Bathsheba
mkewe, akaingia kwake akakutana naye
kimwili. Akazaa mwana, wakamwita
jina lake Solomoni. BWANA alimpenda
Solomoni. 25 [d]Kwa kuwa BWANA alimpenda,
akatuma neno kwa Daudi kwa kinywa cha
nabii Nathani kuwa mtoto aitwe Yedidia[e]
kwa ajili ya BWANA.
26 [f]Wakati huo Yoabu akapigana dhidi ya
Raba jamii ya Waamoni na kuteka ngome la
kifalme. 27 Kisha Yoabu akatuma wajumbe
kwa Daudi, kusema, “Nimepigana dhidi ya
Raba, nami nimetwaa chanzo chake cha
maji. 28 Sasa kusanya vikosi vilivyobaki na
ukauzingire mji kwa jeshi na kuuteka. La
sivyo, nitauteka mimi, nao utaitwa kwa
jina langu.”
29 Kwa hiyo Daudi akakusanya jeshi lote
akaenda Raba, akaushambulia na kuuteka.
30 [g]Akachukua taji kutoka kwa kichwa cha
mfalme wao, lililokuwa na uzito wa talanta
moja ya dhahabu,[h] nayo ilizungushiwa vito
vya thamani. Ikawekwa juu ya kichwa cha
Daudi. Alichukua nyara nyingi kutoka mjini
huo. 31 [i]Akawatoa watu waliokuwa humo,
akawaweka wafanye kazi kwa misumeno,
sululu za chuma na mashoka, naye
akawaweka kwenye kazi ya kutengeneza
matofali. Akafanya hivi kwa miji yote ya
Waamoni. Kisha Daudi na jeshi lake lote
wakarudi Yerusalemu.

*Amnoni Na Tamari*

13 [j]Ikawa baada ya hayo, Amnoni mwana
wa Daudi akampenda Tamari, umbu
lake Absalomu mwana wa Daudi, ambaye
alikuwa mzuri wa sura.
2 Amnoni akasumbuka sana kuhusu
Tamari hata akaugua, kwa kuwa Tamari
alikuwa bikira, na ilionekana kwamba
haiwezekani Amnoni kumfanyia jambo
lolote.
3 [k]Basi Amnoni alikuwa na rafiki jina lake
Yonadabu mwana wa Shimea,[l] nduguye
Daudi. Yonadabu alikuwa mtu wa hila
nyingi sana. 4 [m]Akamuuliza Amnoni, “Wewe
ni mtoto wa mfalme; kwa nini siku baada ya
siku unaonekana kukonda? Hutaniambia?”
Amnoni akamwambia, “Ninampenda
Tamari, dada yake Absalomu ndugu yangu.”
5 Yonadabu akamwambia, “Nenda
ukalale kitandani na ujifanye kuwa
mgonjwa. Baba yako atakapokuja kukuona
mwambie, ‘Ningependa Tamari dada yangu
aje kunipatia chochote ili nile. Tafadhali
mruhusu aje na kuniandalia chakula mbele
yangu ningali ninamwona, ili nipate kula
kutoka mkononi mwake.’ ”
6 [n]Kwa hiyo Amnoni akalala kitandani
kujifanya mgonjwa. Mfalme alipokuja
kumwona, Amnoni akamwambia,
“Ningependa dada yangu Tamari aje na
kuniandalia mikate maalum mbele yangu,
ili nipate kula toka mkononi mwake.”
7 Daudi akampelekea Tamari ujumbe
huko kwenye jumba la kifalme, kusema:
“Nenda katika nyumba ya ndugu yako
Amnoni ukamwandalie chakula.” 8 Kwa
hiyo Tamari akaenda nyumbani kwa
nduguye Amnoni, ndugu ambaye alikuwa
amelala. Tamari akachukua unga uliotiwa
chachu akaukanda, akaiandaa mikate mbele
yake na kuioka. 9 [o]Tamari akaondoa mikate

[a]**12:22** Yon 3:4; Isa 38:1-5
[b]**12:23** Mwa 37:35; 1Sam 31:13; 2Sam 13:39; Ay 7:10; 10:21; 2Kor 5:1-8; Ebr 11:10; 13:14
[c]**12:24** 1Fal 1:10-11; 1Nya 22:9; 28:5; Mt 1:6
[d]**12:25** Neh 13:26
[e]25 Yedidia maana yake Apendwaye na BWANA.
[f]**12:26** Kum 3:11; 1Nya 20:1-3
[g]**12:30** Es 8:15; Za 21:3; 132:18; 1Nya 20:2
[h]30 Talanta moja ya dhahabu ni sawa na kilo 34.
[i]**12:31** 1Sam 14:47
[j]**13:1** 2Sam 3:2; 14:27; 1Nya 3:9; 2Sam 3:3
[k]**13:3** 1Sam 16:9; 1Nya 2:13
[l]3 Shimea pia hutamkwa Shama.
[m]**13:4** Isa 3:9; Eze 23:16
[n]**13:6** Mwa 18:6
[o]**13:9** Mwa 45:1; Amu 3:19; Yn 3:20

kwenye kikaango ili ampatie Amnoni, lakini
akakataa kula.
Amnoni akamwambia, “Mtoe nje kila
mtu aliyeko hapa.” Kwa hiyo kila mmoja
akaondoka. 10 Ndipo Amnoni akamwambia
Tamari, “Leta mkate hapa ndani ya chumba
changu ili nipate kula kutoka mkononi
mwako.” Basi Tamari akachukua mikate
aliyoiandaa na kumletea Amnoni ndugu
yake ndani ya chumba chake. 11 [a]Lakini
alipompelekea ili ale, akamkamata kwa
nguvu na kumwambia, “Njoo ulale nami,
dada yangu.”
12 [b]Akamwambia, “Usifanye hivyo, ndugu
yangu! Usinitende jeuri! Jambo la namna
hii halistahili kufanyika katika Israeli!
Usitende jambo hili ovu. 13 [c]Kwa upande
wangu je, itakuwaje? Nitaipeleka wapi aibu
yangu? Pia kwa upande wako, itakuwaje?
Utakuwa kama mmoja wa wapumbavu
waovu katika Israeli. Tafadhali zungumza
na mfalme; hatakukatalia wewe kunioa,”
14 [d]Lakini Amnoni akakataa kumsikiliza, na
kwa kuwa alikuwa na nguvu kuliko Tamari,
akamtenda jeuri.
15 Kisha Amnoni akamchukia Tamari,
kwa machukio makuu sana. Kwa kweli,
Amnoni alimchukia kuliko alivyokuwa
amempenda. Amnoni akamwambia, “Inuka
na utoke nje!”
16 Tamari akamwambia, “Hapana!
Kunifukuza itakuwa vibaya zaidi kuliko
yale uliyonitendea.”
Lakini Amnoni akakataa kumsikiliza.
17 Akamwita mtumishi wake mahsusi na
kumwambia, “Mtoe huyu mwanamke
hapa na ufunge mlango nyuma yake.”
18 [e]Kwa hiyo, mtumishi wake akamtoa nje
na kufunga mlango nyuma yake. Tamari
alikuwa amevaa joho lililopambwa
vizuri, kwa maana lilikuwa aina ya
mavazi yaliyovaliwa na binti za mfalme
waliokuwa mabikira. 19 [f]Tamari akajitia
majivu kichwani mwake na kurarua lile
joho alilokuwa amevaa. Akaweka mkono
wake kichwani, akaenda zake akilia kwa
sauti.
20 Absalomu nduguye akamuuliza, “Je,
huyo Amnoni ndugu yako, amekutana
nawe kimwili? Sasa nyamaza umbu langu,
yeye ni ndugu yako. Usilitie jambo hili
moyoni.” Naye Tamari akaishi nyumbani
kwa Absalomu nduguye, akiwa mwanamke
mwenye huzuni.
21 [g]Mfalme Daudi aliposikia mambo
haya yote, akakasirika sana. 22 [h]Absalomu
hakusema neno lolote na Amnoni, likiwa
zuri au baya, kwa kuwa alimchukia Amnoni
kwa sababu alikuwa amemtia aibu Tamari,
dada yake.

*Absalomu Amuua Amnoni*

23 [i]Miaka miwili baadaye, wakati
wakata manyoya ya kondoo wa Absalomu
walipokuwa huko Baal-Hasori karibu na
mpaka wa Efraimu, alialika wana wote wa
mfalme kuja huko. 24 Absalomu akaenda
kwa mfalme na kumwambia, “Mtumishi
wako ninao wakata manyoya ya kondoo
waliokuja. Tafadhali, je, mfalme na maafisa
wake wanaweza kuungana nami?”
25 Mfalme akajibu, “La hasha, mwanangu
si lazima sisi sote tuje, tutakuwa tu mzigo
kwako.” Ingawa Absalomu alimsihi sana,
mfalme alikataa kwenda, lakini alimbariki.
26 Basi Absalomu akasema, “Kama
hutakuja, tafadhali mruhusu ndugu yangu
Amnoni twende pamoja naye.”
Mfalme akamuuliza, “Kwa nini aende
pamoja nawe?” 27 Lakini Absalomu alimsihi,
kwa hiyo mfalme akamtuma Amnoni
pamoja na wana wengine wa mfalme
waliobaki.

[a] **13:11** Mwa 39:12; Mit 7:13; Mhu 7:26; Mwa 38:19
[b] **13:12** Law 20:17; Amu 20:6; 19:23; Law 18:19; Mwa 34:7; Mit 7:7-23
[c] **13:13** Law 18:9; Kum 22:21-24; Mwa 19:8; Amu 19:24
[d] **13:14** Mwa 34:2; Eze 22:11; Kum 22:25; Law 18:19; 20:17; Amu 20:5; 2Sam 12:11
[e] **13:18** Mwa 37:23; Amu 5:30; Za 45:14
[f] **13:19** Yos 7:6; Es 4:1; Dan 9:3; 2Sam 1:2; Ay 2:12; 42:6; Yer 2:37
[g] **13:21** Mwa 34:7
[h] **13:22** Mwa 31:24; Law 19:17-18; 1Yn 2:9-11; Mit 10:18; Efe 4:26, 31
[i] **13:23** 1Sam 25:7; Mwa 38:12; 1Fal 3:4; Yos 17:18; Amu 7:24

28 [a]Absalomu aliagiza watu wake,
"Sikilizeni! Wakati Amnoni atakapokuwa
amekunywa mvinyo na kulewa sana nami
nikiwaambia, 'Mpigeni Amnoni,' basi
muueni. Msiogope. Je, si mimi niliyewapa
amri hii? Kuweni hodari na wenye
ushujaa." 29 Kwa hiyo watu wa Absalomu
wakamtendea Amnoni kama vile Absalomu
alivyokuwa amewaagiza. Ndipo wana wote
wa mfalme wakainuka, wakapanda nyumbu
zao, wakakimbia.
30 Wakati wakiwa njiani, taarifa ilimjia
Daudi, kusema: "Absalomu amewaua wana
wote wa mfalme; hakuna hata mmoja
aliyesalia." 31 [b]Mfalme akasimama, akararua
nguo zake, akalala chini ardhini; nao
watumishi wake wote wakasimama kando
yake na nguo zao zikiwa zimeraruliwa.
32 Lakini Yonadabu mwana wa Shimea,
nduguye Daudi, akasema, "Bwana wangu
asifikiri kwamba wamewaua wana wote wa
mfalme; ni Amnoni peke yake ndiye alikufa.
Hili limekuwa kusudi la moyo wa Absalomu
tangu siku ile Amnoni alipomtendea jeuri
Tamari, dada yake. 33 [c]Mfalme bwana
wangu asisumbuliwe na taarifa kwamba
wamewaua wana wote wa mfalme. Ni
Amnoni peke yake aliyekufa."
34 Wakati huo, Absalomu akawa
amekimbia.

Basi mlinzi akaangalia, naye akaona watu wengi barabarani magharibi yake, wakishuka kutoka upande wa kilima. Mlinzi akaenda akamwambia mfalme, "Naona watu wakitokea upande wa Horonaimu, huko upande wa kilimani."

35 Yonadabu akamwambia mfalme,
"Tazama, wana wa mfalme wako hapa;
imekuwa kama vile mtumishi wako
alivyosema."
36 Mara alipomaliza kusema, wana wa
mfalme wakaingia ndani wakiomboleza
kwa makelele. Pia mfalme na watumishi
wake wote wakalia sana kwa uchungu.

37 [d]Absalomu akakimbia na kwenda kwa
Talmai mwana wa Amihudi, mfalme wa
Geshuri. Lakini Mfalme Daudi akaomboleza
kwa ajili ya mwanawe kila siku.
38 [e]Baada ya Absalomu kukimbia na
kwenda Geshuri, akakaa huko miaka
mitatu. 39 [f]Roho ya Mfalme Daudi ikatamani
kumwendea Absalomu, kwa maana mfalme
alikuwa amefarijika kuhusu kifo cha
Amnoni.

*Absalomu Arudi Yerusalemu*

14 [g]Yoabu mwana wa Seruya akafahamu
kuwa moyo wa mfalme ulikuwa na
shauku ya kumwona Absalomu. 2 [h]Kwa
hiyo Yoabu akamtuma mtu fulani kwenda
Tekoa na kumleta mwanamke mwenye
hekima kutoka huko. Akamwambia
huyo mwanamke, "Jifanye uko katika
maombolezo. Vaa nguo za kuomboleza,
nawe usitumie mafuta yoyote ya uzuri,
jifanye kama mwanamke ambaye amekuwa
na huzuni kwa siku nyingi kwa ajili
ya kufiwa. 3 [i]Kisha nenda kwa mfalme
ukazungumze maneno haya." Naye Yoabu
akaweka maneno kinywani mwa yule
mwanamke.
4 [j]Huyo huyo mwanamke kutoka Tekoa
alipofika kwa mfalme, akaanguka kifudifudi
kumpa mfalme heshima, akasema, "Ee
mfalme, nisaidie!"
5 [k]Mfalme akamuuliza, "Una shida gani?"

Akamwambia, "Mimi ni mjane hasa,
mume wangu amekufa. 6 Mimi mtumishi
wako nilikuwa na wana wawili. Wakapigana
wao kwa wao huko shambani wala
huko hapakuwa na mtu hata mmoja wa
kuwaamua. Mmoja akampiga mwenzake na
kumuua. 7 [l]Sasa ukoo wote umeinuka dhidi

[a]**13:28** 2Sam 3:3; Rut 3:7; 2Sam 12:10; Amu 19:6-9, 22; 1Sam 25:36; Mwa 9:21; 19:32-35; Es 1:10; Za 104:15
[b]**13:31** Hes 14:6; 2Sam 1:11; Mwa 37:29; 2Sam 12:16
[c]**13:33** 2Sam 19:19
[d]**13:37** 2Sam 3:3; 14:23-32; 1Nya 3:2
[e]**13:38** 2Sam 14:23; 15:8
[f]**13:39** 2Sam 14:13; 12:19-23; Mwa 38:12
[g]**14:1** 2Sam 2:18
[h]**14:2** Neh 3:5; Yer 6:1; Amo 1:1; 2Sam 20:16; Rut 3:3; Isa 1:6; 2Nya 11:6; 20:20
[i]**14:3** Kut 4:15
[j]**14:4** 1Sam 20:41; 2Sam 1:2; 2Fal 6:26
[k]**14:5** 2Sam 12:1
[l]**14:7** Hes 35:19; Mt 21:38; Kum 19:10-13; Mwa 4:14

ya mtumishi wako, wakisema, 'Utukabidhi
huyo aliyemuua ndugu yake, ili tumuue
kwa ajili ya uhai wa ndugu yake ambaye
alimuua, nasi hapo tutakuwa tumekatilia
mbali na mrithi pia.' Wakifanya hivyo,
watakuwa wamezima tumaini langu
lililobaki, mume wangu hataachiwa jina
wala mzao katika uso wa dunia."
8 [a]Mfalme akamwambia huyo mwanamke,
"Nenda nyumbani, nami nitatoa agizo kwa
ajili yako."
9 [b]Lakini huyo mwanamke kutoka Tekoa
akamwambia, "Mfalme bwana wangu,
lawama na iwe juu yangu na juu ya nyumba
ya baba yangu, naye mfalme na kiti chake
cha enzi na asiwe na hatia."
10 Mfalme akajibu, "Ikiwa mtu yeyote
atakusemesha lolote, mlete kwangu, naye
hatakusumbua tena."
11 [c]Huyo mwanamke akasema, "Basi
mfalme na amwombe BWANA Mungu wake
ili kuzuia mlipiza kisasi cha damu kuongeza
juu ya uharibifu, ili kwamba mwanangu
asije akaangamizwa."
Mfalme akasema, "Hakika kama aishivyo
BWANA, hakuna unywele mmoja wa kichwa
cha mwanao utakaoanguka chini."
12 Ndipo huyo mwanamke akasema,
"Mruhusu mtumishi wako aseme neno kwa
mfalme bwana wangu."
Mfalme akajibu, "Sema."
13 [d]Huyo mwanamke akasema, "Mbona
basi wewe umewaza jambo kama hili dhidi
ya watu wa Mungu? Je, mfalme asemapo
hili, hajitii hatiani mwenyewe, kwa
maana mfalme hajamrudisha mwanawe
aliyefukuziwa mbali? 14 [e]Kama vile maji
yaliyomwagika ardhini, yasivyoweza
kuzoleka tena, hivyo sisi kufa ni lazima.
Lakini Mungu haondoi uhai, badala yake,
yeye hufanya njia ili kwamba aliyefukuzwa
asibaki akiwa amefarikishwa naye.
15 "Nami sasa nimekuja kusema hili
kwa bwana wangu mfalme kwa sababu
watu wameniogopesha. Mtumishi wako
alifikiri, 'Nitanena na mfalme, labda
mfalme atamfanyia mtumishi wake kile
anachoomba. 16 [f]Labda mfalme atakubali
kumwokoa mtumishi wake kutoka mkononi
mwa mtu anayejaribu kunikatilia mbali,
mimi na mwanangu, kutoka kwenye urithi
Mungu aliotupatia.'
17 [g]"Basi sasa mtumishi wako anasema,
'Neno la bwana wangu mfalme na linipatie
pumziko, kwa maana bwana wangu
mfalme ni kama malaika wa Mungu katika
kutambua jema na baya. BWANA Mungu
wako na awe pamoja nawe.' "
18 Basi mfalme akamwambia huyo
mwanamke, "Usinifiche jibu kuhusu hilo
nitakalokuuliza."
Huyo mwanamke akasema, "Mfalme
bwana wangu na aseme."
19 Mfalme akauliza, "Je, mkono wa
Yoabu haupo pamoja nawe katika jambo
hilo lote?"
Huyo mwanamke akajibu, "Hakika kama
uishivyo, bwana wangu mfalme, hakuna
yeyote anayeweza kugeuka kulia wala
kushoto kutokana na chochote anachosema
bwana wangu mfalme. Naam, ni mtumishi
wako Yoabu ndiye alinifundisha kufanya
hivi, naye ndiye aliweka maneno haya yote
kinywani mwa mtumishi wako. 20 [h]Mtumishi
wako Yoabu amefanya hivi ili kubadili hali
iliyopo. Bwana wangu ana hekima kama ile
ya malaika wa Mungu, hufahamu kila kitu
kinachotokea katika nchi."
21 Mfalme akamwambia Yoabu, "Vyema
sana, nitalifanya jambo hili. Nenda,
ukamlete kijana Absalomu."
22 [i]Yoabu akaanguka kifudifudi mpaka
ardhini kumpa mfalme heshima, naye

[a]**14:8** 1Sam 25:35
[b]**14:9** 1Sam 25:24; Mt 27:25; 1Sam 25:28; 1Fal 2:33; Mwa 27:13; 2Sam 3:28-29; Hes 35:33
[c]**14:11** Hes 35:12; Mt 10:30; 1Sam 14:45; Yos 20:3-6; 1Sam 28:10; Mdo 27:34
[d]**14:13** 2Sam 12:7; 1Fal 20:40; 2Sam 13:38-39; Amu 20:2
[e]**14:14** Ay 14:11; Za 58:7; Isa 19:5; Ay 10:8; 17:13; 30:23; Za 22:15; Ebr 9:27; Hes 35:15-28; Mhu 3:19
[f]**14:16** Kut 34:9; 1Sam 26:19
[g]**14:17** 1Sam 29:9; 1Fal 3:9; Dan 2:21; 2Sam 19:27
[h]**14:20** 1Fal 3:21; 10:23-24; Isa 28:6; 2Sam 18:13; 19:27
[i]**14:22** Mwa 47:7

akambariki mfalme. Yoabu akasema, “Leo
mtumishi wako anajua kuwa amepata kibali
machoni pako, bwana wangu mfalme, kwa
sababu mfalme amemjalia mtumishi wake
ombi lake.”
23 [a]Ndipo Yoabu akaenda hadi Geshuri
akamrudisha Absalomu Yerusalemu.
24 [b]Lakini mfalme akasema, “Lazima
Absalomu aende kwenye nyumba yake
mwenyewe; kamwe asiuone uso wangu.”
Kwa hiyo Absalomu akaenda kwenye
nyumba yake na hakuuona uso wa mfalme.
25 [c]Katika Israeli yote hakuna mtu yeyote
aliyesifiwa kwa uzuri wa sura kama
Absalomu. Kuanzia utosi wa kichwa chake
hadi wayo wa mguu wake hapakuwa na
kasoro. 26 [d]Kila mara aliponyoa nywele za
kichwa chake, kwa kuwa alikuwa akinyoa
mara kwa mara zilipokuwa zinamwia nzito,
alizipima uzito wake ulikuwa shekeli mia
mbili kwa kipimo cha kifalme.[e]
27 [f]Walizaliwa wana watatu na binti
mmoja kwa Absalomu. Jina la binti yake
aliitwa Tamari, naye akawa mwanamke
mzuri wa sura.
28 Absalomu akaishi miaka miwili huko
Yerusalemu pasipo kuuona uso wa mfalme.
29 Basi Absalomu akamwita Yoabu kwa
kusudi la kumtuma kwa mfalme, lakini
Yoabu akakataa kuja kwa Absalomu.
Ndipo akamwita tena mara ya pili, lakini
pia akakataa kuja. 30 [g]Ndipo akawaambia
watumishi wake, “Tazama, shamba la
Yoabu liko jirani na langu, naye ana shayiri
humo. Nendeni mkalitie moto.” Kisha
watumishi wa Absalomu wakalitia moto
shamba hilo.
31 [h]Basi Yoabu akaenda nyumbani kwa
Absalomu, akamwambia, “Kwa nini
watumishi wako wametia moto shamba
langu?”
32 [i]Absalomu akamwambia Yoabu,
“Tazama, nilikutumia ujumbe na kusema,
‘Njoo ili niweze kukutuma kwa mfalme
kuuliza, “Kwa nini nimekuja kutoka
Geshuri? Ingekuwa bora zaidi kwangu
kama ningebaki huko!” ’ Sasa basi, nataka
kuuona uso wa mfalme, na ikiwa nina hatia
ya jambo lolote, basi na aniue.”
33 [j]Basi Yoabu akaenda kwa mfalme na
kumwambia jambo hili. Kisha mfalme
akamwita Absalomu, naye akaingia ndani
akasujudu uso wake mpaka ardhini mbele
ya mfalme. Naye mfalme akambusu
Absalomu.

### *Mipango Ya Hila Ya Absalomu*

15 [k]Baada ya muda, Absalomu akajipatia
magari ya vita na farasi pamoja na
watu hamsini wa kupiga mbio mbele yake.
2 [l]Akawa anaamka asubuhi na mapema na
kusimama kando ya barabara inayoelekea
kwenye lango la mji. Wakati wowote
alipokuja mtu yeyote mwenye mashtaka
yanayohitaji kuletwa mbele ya mfalme kwa
maamuzi, Absalomu naye angemwita na
kumuuliza, “Wewe unatoka mji upi?” Naye
angejibu, “Mtumishi wako anatoka katika
mojawapo ya makabila ya Israeli.” 3 [m]Kisha
Absalomu angemwambia, “Tazama,
malalamiko yako ni ya haki na sawasawa,
lakini hakuna mwakilishi wa mfalme wa
kukusikiliza.” 4 [n]Absalomu aliongeza, “Laiti
tu ningeteuliwa kuwa mwamuzi katika
nchi. Ndipo kila mmoja mwenye mashtaka
au shauri angekuja kwangu nami ningeona
kwamba anapata haki.”
5 [o]Pia, wakati mtu yeyote alipomkaribia
ili kusujudu mbele yake, Absalomu
alinyoosha mkono wake na kumshika pia

[a]**14:23** Kum 3:14; 2Sam 3:3; 13:37
[b]**14:24** Mwa 43:3; 2Sam 3:13; Ufu 22:4
[c]**14:25** Kum 28:35; Ay 2:7; Isa 1:6; Efe 5:27
[d]**14:26** 2Sam 18:9; Eze 44:20
[e]26 Shekeli 200 kwa kipimo cha kifalme ni sawa na kilo 2.3.
[f]**14:27** 2Sam 18:18; 13:1
[g]**14:30** Kut 9:31; 2Sam 13:28; Amu 15:5
[h]**14:31** Amu 15:5
[i]**14:32** 2Sam 3:3; 1Sam 20:8; Ay 31:33; Mit 28:13; Yer 8:12
[j]**14:33** Lk 15:20; Mwa 33:4; 45:15
[k]**15:1** 2Sam 12:11; 1Sam 8:11; 1Fal 1:5; Mit 11:2; 16:18
[l]**15:2** Mwa 23:10; 2Sam 19:8; Mit 1:16
[m]**15:3** Mit 12:2
[n]**15:4** Rum 16:18; Amu 9:29
[o]**15:5** Za 12:2

kumbusu. [6] [a]Absalomu akaendelea na tabia
hii mbele ya Waisraeli wote waliomjia
mfalme kumwomba awape haki; kwa hiyo
Absalomu akaiba mioyo ya watu wa Israeli.
[7] [b]Mnamo mwisho wa mwaka wa nne,
Absalomu akamwambia mfalme, "Naomba
unipe ruhusa niende Hebroni nikatimize
nadhiri niliyomwekea BWANA. [8] [c]Wakati
mtumishi wako alipokuwa huko Geshuri
katika nchi ya Aramu, niliweka nadhiri hii,
'Ikiwa BWANA atanirudisha Yerusalemu,
nitamwabudu BWANA huko Hebroni.' "
[9] Mfalme akamwambia, "Enenda kwa
amani." Hivyo akaenda Hebroni.
[10] [d]Kisha Absalomu akatuma wajumbe
kwa siri katika makabila yote ya Israeli,
kusema, "Mara mtakaposikia sauti ya
tarumbeta basi semeni, 'Absalomu ni
mfalme huko Hebroni.' " [11] [e]Watu mia mbili
kutoka Yerusalemu walikuwa wamefuatana
na Absalomu. Walikuwa wamealikwa kama
wageni nao walikwenda kwa nia njema,
pasipo kujua lolote. [12] [f]Wakati Absalomu
alipokuwa anatoa dhabihu, pia akatuma
aitwe Ahithofeli, Mgiloni, mshauri wa
Daudi, aje kutoka Gilo, ambao ndio mji
wake wa nyumbani. Kwa hiyo mpango
wa hila ukapata nguvu, na idadi ya
waliofuatana na Absalomu ikaongezeka.

*Kukimbia Kwa Daudi*

[13] [g]Mjumbe akaja na kumwambia Daudi,
"Mioyo ya watu wa Israeli inaambatana na
Absalomu."
[14] [h]Ndipo Daudi akawaambia maafisa
wake wote waliokuwa pamoja naye
huko Yerusalemu, "Njooni! Ni lazima
tukimbie, la sivyo hakuna hata mmoja
wetu atakayeokoka kutoka mkononi
mwa Absalomu. Ni lazima tuondoke kwa
haraka, la sivyo atakuja mbio na kutupata,
atatuangamiza na kuupiga mji kwa upanga."
[15] Maafisa wa mfalme wakamjibu,
"Watumishi wako tu tayari kufanya lolote
mfalme bwana wetu analochagua."
[16] [i]Mfalme akatoka, pamoja na watu
wa nyumbani mwake wakimfuata; lakini
akawaacha masuria kumi ili kuangalia jumba
la kifalme. [17] Hivyo mfalme akaondoka,
pamoja na watu wote wakimfuata,
wakatua mahali mbali kiasi. [18] [j]Watu wake
wote wakatembea, wakampita wakiwa
wamefuatana na Wakerethi na Wapelethi
wote; pia Wagiti wote mia sita waliokuwa
wamefuatana naye kutoka Gathi wakapita
mbele ya mfalme.
[19] [k]Mfalme akamwambia Itai, Mgiti, "Kwa
nini ufuatane na sisi? Rudi ukakae pamoja
na Mfalme Absalomu. Wewe ni mgeni,
mkimbizi kutoka nchini mwako. [20] [l]Ulikuja
jana tu. Nami leo nikufanye utangetange
pamoja nasi, wakati sijui niendako? Rudi,
nawe ukawachukue watu wa kwenu. Wema
na uaminifu na viwe pamoja nawe."
[21] [m]Lakini Itai akamjibu mfalme, "Hakika
kama BWANA aishivyo na kama mfalme
bwana wangu aishivyo, popote mfalme
bwana wangu atakapokuwa, ikiwa ni
kuishi au kufa, hapo ndipo mtumishi wako
atakapokuwa."
[22] Daudi akamwambia Itai, "Songa mbele,
endelea." Kwa hiyo Itai, Mgiti, akaendelea
pamoja na watu wake wote, pia jamaa zote
waliokuwa pamoja naye.
[23] [n]Watu wote wa nje ya mji wakalia
kwa sauti wakati watu wote walipokuwa
wakipita. Mfalme naye akavuka Bonde

[a]**15:6** 2Sam 3:3; Mwa 28:20; 2Sam 13:37-38; Rum 16:18
[b]**15:7** 2Sam 2:1
[c]**15:8** 1Fal 1:34, 39; 2Fal 9:13; 1Sam 16:2; Mwa 28:20; 1Sam 1:11; Za 56:12; 2Sam 13:38
[d]**15:10** 1Fal 1:34, 39; 2Fal 9:13
[e]**15:11** 1Sam 9:13; 16:3-5; Mwa 20:5; Mit 14:15; Mt 10:16; Rum 16:18-19
[f]**15:12** 2Sam 16:15, 23; 17:14; 23:34; 1Nya 27:33; Ay 19:14; Za 41:9; 55:13; Yer 9:4; Yos 15:51; Za 3:1; Mik 7:5-6
[g]**15:13** Amu 9:3
[h]**15:14** 1Fal 2:26; Za 132:1; 3; 2Sam 16:9
[i]**15:16** 2Sam 16:21-22; 20:3; 12:11
[j]**15:18** 1Sam 30:14; 2Sam 20:7, 23; 1Fal 1:34, 44; 1Nya 18:17; 2Sam 8:18
[k]**15:19** 2Sam 18:2; Mwa 31:15
[l]**15:20** 1Sam 22:2; 2:6; 23:13
[m]**15:21** Rut 1:16-17; Mit 17:17; 1Sam 20:3; 2Fal 2:2-6
[n]**15:23** 1Sam 11:4; Ay 2:12; 1Fal 2:37; 2Fal 23:12; 2Nya 15:16; 29:16; 30:14; Yer 31:40; Yn 18:1; 2Sam 16:2; Mt 3:1-3

la Kidroni, nao watu wote wakaelekea
jangwani.
24 [a]Sadoki pia alikuwako, kadhalika
Walawi wote waliokuwa pamoja naye
walikuwa wamechukua Sanduku la Agano
la Mungu. Wakaweka chini Sanduku la
Mungu, naye Abiathari akatoa dhabihu
mpaka watu wote walipokuwa wameondoka
mjini.
25 [b]Kisha mfalme akamwambia Sadoki,
“Rudisha Sanduku la Mungu mjini.
Ikiwa nitapata kibali mbele za BWANA,
atanirudisha, nami nitaliona Sanduku hili
tena pamoja na Maskani yake. 26 [c]Lakini
kama yeye atasema, ‘Mimi sipendezwi
nawe,’ basi mimi niko tayari; yeye na
anifanye chochote aonacho chema kwake.”
27 [d]Pia mfalme alimwambia kuhani
Sadoki, “Je, wewe si mwonaji? Rudi mjini
kwa amani pamoja na mwanao Ahimaasi
na Yonathani mwana wa Abiathari. Wewe
na Abiathari wachukueni wana wenu
wawili. 28 [e]Nitasubiri kwenye vivuko katika
jangwa mpaka neno litakapotoka kwenu
kuniarifu.” 29 Kwa hiyo Sadoki na Abiathari
wakarudisha Sanduku la Mungu mpaka
Yerusalemu na kukaa huko.
30 [f]Bali Daudi akaendelea, akapanda
Mlima wa Mizeituni, akaenda huku analia,
akiwa amefunika kichwa chake na bila viatu
miguuni. Watu wote waliokuwa pamoja
naye nao wakafunika vichwa vyao, wakawa
wanapanda mlima huku wanalia. 31 [g]Basi
Daudi alikuwa ameambiwa, “Ahithofeli
alikuwa miongoni mwa washiriki wa shauri
baya la Absalomu.” Ndipo Daudi akaomba,
akisema, “Ee BWANA, geuza shauri la
Ahithofeli kuwa ujinga.”
32 [h]Daudi alipofika kwenye kilele cha
mlima, mahali ambapo watu walikuwa
wamezoea kumwabudu Mungu, Hushai,
Mwariki, alikuwako huko kumlaki, joho
lake likiwa limeraruka na mavumbi
kichwani mwake. 33 [i]Daudi akamwambia,
“Kama ukienda pamoja nami, utakuwa
mzigo kwangu. 34 [j]Lakini ikiwa utarudi
mjini na kumwambia Absalomu, ‘Nitakuwa
mtumishi wako, ee mfalme; nilikuwa
mtumishi wa baba yako wakati uliopita,
lakini sasa nitakuwa mtumishi wako,’ basi
utaweza kunisaidia kwa kupinga shauri
la Ahithofeli. 35 [k]Je, makuhani Sadoki na
Abiathari hawatakuwa pamoja nawe?
Waambie lolote utakalosikia katika jumba
la mfalme. 36 [l]Wana wao wawili, Ahimaasi
mwana wa Sadoki na Yonathani mwana wa
Abiathari, wako pamoja nao huko. Watume
kwangu na lolote utakalosikia.”
37 [m]Kwa hiyo Hushai, rafiki wa Daudi,
akafika Yerusalemu wakati Absalomu
alipokuwa anaingia mjini.

*Daudi Na Siba*

16 [n]Daudi alipokuwa amekwenda
umbali mfupi kupita kilele cha
mlima, akamkuta huko Siba, msimamizi
wa shughuli za Mefiboshethi, akingojea
kumlaki Daudi. Alikuwa na punda wawili
wakiwa wametandikwa na kupakiwa mikate
mia mbili, maandazi mia ya zabibu kavu,
maandazi mia ya tini na kiriba cha divai.
2 [o]Mfalme Daudi akamuuliza Siba, “Kwa
nini umeleta vitu hivi?”
Siba akamjibu, “Punda ni kwa ajili ya
watu wa nyumba ya mfalme kupanda,
mikate na matunda ni kwa ajili ya watu

[a]**15:24** 2Sam 8:17; 19:11; Hes 4:18; 10:33; 1Fal 2:26; 1Sam 22:20
[b]**15:25** Kut 15:13; Law 15:31; Za 43:3; 46:4; 84:1; 132:7; 2Sam 6:17
[c]**15:26** Amu 10:15; 2Sam 22:20; 1Fal 10:9; Hes 14:8; 2Nya 9:8; Isa 62:4; 1Sam 3:18
[d]**15:27** 1Sam 9:9; 2Sam 17:17; 1Fal 1:42; 2Sam 24:11
[e]**15:28** 2Sam 17:16
[f]**15:30** Hes 25:6; Za 30:5; Es 6:12; Isa 20:2-4; Zek 14:4; Mt 21:1; Lk 19:20; Mdo 1:12; Yer 14:3; Za 126:6; Mt 5:4; Rum 12:15
[g]**15:31** 2Sam 16:23; 17:14, 23; Za 3:1; 55:12
[h]**15:32** 2Sam 16:16; 17:5; 1Fal 4:16; Yos 16:2; 7:6; 2Sam 1:2
[i]**15:33** 2Sam 19:35
[j]**15:34** 2Sam 16:19; 17:14; Mit 11:14
[k]**15:35** 2Sam 17:15-16
[l]**15:36** 2Sam 18:19; 17:17; 1Fal 1:42
[m]**15:37** 1Nya 27:33; 2Sam 16:15-17; Mit 17:17
[n]**16:1** 2Sam 9:1-3; 1Sam 25:18; 1Nya 12:40; 2Sam 15:30
[o]**16:2** 2Sam 17:27-29; Amu 5:10; 10:4; 1Sam 25:27; 2Sam 15:23; Mit 15:23; 31:6; Za 104:15; 1Tim 5:23

kula, nayo divai ni kwa kuwaburudisha
watakaochoka jangwani."
3 [a]Kisha mfalme akauliza, "Yuko wapi
mwana wa bwana wako?"

Siba akamwambia, "Anakawia
Yerusalemu, kwa sababu anafikiri, 'Leo
nyumba ya Israeli itanirudishia utawala
wa baba yangu.' "
4 [b]Ndipo mfalme akamwambia Siba, "Yote
yaliyokuwa mali ya Mefiboshethi sasa ni
mali yako."

Siba akasema, "Nasujudu kwa
unyenyekevu. Naomba nipate kibali mbele
yako, bwana wangu mfalme."

*Shimei Amlaani Daudi*

5 [c]Mfalme Daudi alipokuwa anakaribia
Bahurimu, mtu mmoja kutoka ukoo huo
huo kama jamaa ya Sauli, akatoka humo,
ambaye jina lake ni Shimei mwana wa
Gera; akawa analaani alipokuwa akitoka.
6 Akamtupia Daudi na maafisa wote wa
mfalme mawe, ingawa vikosi vyote na
walinzi maalum walikuwa kulia na kushoto
mwa Daudi. 7 Shimei alivyokuwa akilaani,
akasema, "Toka hapa, toka hapa, wewe
mtu wa damu, wewe mtu mbaya kabisa!
8 [d]BWANA amekulipiza kwa ajili ya damu
yote uliyomwaga ya watu wa nyumba
ya Sauli, ambaye nafasi yake umeimiliki
wewe. BWANA amekabidhi ufalme mkononi
mwa mwanao Absalomu. Maangamizi
yamekupata kwa sababu wewe ni mtu wa
damu!"
9 [e]Ndipo Abishai mwana wa Seruya
akamwambia mfalme, "Kwa nini huyu
mbwa mfu amlaani bwana wangu mfalme?
Niruhusu nivuke nikatilie mbali kichwa
chake."
10 [f]Lakini mfalme akamwambia, "Mna
nini nami, enyi wana wa Seruya? Ikiwa
analaani kwa sababu BWANA amemwambia,
'Mlaani Daudi,' nani awezaye kuuliza, 'Kwa
nini unafanya hivi?' "
11 [g]Ndipo Daudi akamwambia Abishai
na maafisa wake wote, "Mwanangu,
yeye ambaye ametoka viunoni mwangu
mwenyewe, anajaribu kuuondoa uhai
wangu. Je, si zaidi sana kwa huyu
Mbenyamini! Mwacheni, acha alaani, kwa
maana BWANA amemwambia afanye hivyo.
12 [h]Inawezekana kwamba BWANA ataona
dhiki yangu na kunilipa mema kwa ajili ya
laana ninayopokea leo."
13 Kwa hiyo Daudi na watu wake
wakaendelea na safari yao barabarani,
huku Shimei akiwa anatembea pembezoni
mwa kilima sambamba na Daudi, huku
akimlaani na kumtupia Daudi mawe na
kumrushia mavumbi. 14 [i]Mfalme na watu
wote aliokuwa pamoja nao wakafika
kwenye kituo chao wakiwa wamechoka.
Mfalme akajiburudisha hapo.

*Shauri La Hushai Na Ahithofeli*

15 [j]Wakati huo, Absalomu pamoja na
watu wote wa Israeli wakafika Yerusalemu,
naye Ahithofeli alikuwa pamoja naye.
16 [k]Ndipo Hushai, Mwariki, rafiki wa Daudi,
akamwendea Absalomu na kumwambia,
"Mfalme aishi maisha marefu! Mfalme aishi
maisha marefu!"
17 [l]Absalomu akamuuliza Hushai, "Je, huu
ndio upendo unaomwonyesha rafiki yako?
Kwa nini hukufuatana na rafiki yako?"
18 Hushai akamwambia Absalomu,
"La hasha, yeye aliyechaguliwa na
BWANA, aliyechaguliwa na watu hawa,
atakayechaguliwa tena na watu wote wa
Israeli, huyu ndiye nitakayekuwa wake,
nami nitabakia pamoja naye. 19 [m]Zaidi ya

---

[a]**16:3** 2Sam 9:9-10; 19:26-27
[b]**16:4** 2Sam 4:4; 14:10-11; Mit 18:13
[c]**16:5** 2Sam 3:16; 19:16-23; 1Fal 2:8, 36, 44; Kut 22:28; 2Sam 19:16
[d]**16:8** 2Sam 19:28; 21:9; 19:19; Za 55:3; Amu 9:24; 1Fal 2:32-33; Ufu 16:6
[e]**16:9** 1Sam 26:6; 2Sam 3:8, 39; Lk 9:54; Kut 22:28
[f]**16:10** 2Sam 2:18; 19:22; Rum 9:20; 2Sam 3:39; 1Pet 2:23; 1Fal 18:25; Mao 3:38
[g]**16:11** 2Sam 12:11; Mwa 45:5; 1Sam 26:17
[h]**16:12** Za 4:1; 25:18; Kum 23:5; Rum 8:28; Mwa 29:32; Za 37:7; Yer 24:5-7; Mao 3:22-26; Mt 5:11-12; 2Kor 4:17
[i]**16:14** Za 109:28; 2Sam 17:2
[j]**16:15** 2Sam 15:37; 15:12
[k]**16:16** 2Sam 15:32
[l]**16:17** 2Sam 19:24-25; Mit 17:17; 2Sam 15:32
[m]**16:19** 2Sam 15:34; 1Sam 28:2

hayo, nimtumikie nani? Je, nisimtumikie
mwana? Kama vile nilivyomtumikia baba
yako, ndivyo nitakavyokutumikia wewe.”
20 [a]Absalomu akamwambia Ahithofeli,
“Tupe shauri lako. Tufanye nini?”
21 [b]Ahithofeli akamjibu, “Kutana kimwili
na masuria wa baba yako aliowaacha
kutunza jumba la kifalme. Ndipo Israeli
yote itakaposikia kwamba umejifanya
chukizo kwa baba yako, nayo mikono ya
kila mmoja aliye pamoja nawe itatiwa
nguvu.” 22 [c]Kwa hiyo wakasimika hema
kwa ajili ya Absalomu juu ya paa, naye
akakutana kimwili na masuria wa baba
yake mbele ya Israeli wote.
23 [d]Ilikuwa katika siku hizo shauri
lililotolewa na Ahithofeli lilikuwa kama
lile ambalo limeulizwa kwa Mungu. Ndivyo
Daudi na Absalomu walivyoyaheshimu
mashauri yote ya Ahithofeli.

17 Ahithofeli akamwambia Absalomu,
“Nipe ruhusa niwachague watu kumi
na mbili elfu na waanze safari usiku huu huu
kumfuatia Daudi. 2 [e]Nitamshambulia wakati
akiwa amechoka na ni dhaifu. Nitampiga na
hofu, na kisha watu wote walio pamoja naye
watakimbia. Nitampiga mfalme peke yake
3 [f]na kuwarudisha watu wote kwako. Kifo
cha mtu yule unayemtafuta kitamaanisha
kurudi kwa wote, hakuna hata mtu mmoja
atakayeumizwa.” 4 Mpango huu ulionekana
mzuri kwa Absalomu na kwa wazee wote
wa Israeli.
5 [g]Lakini Absalomu akasema, “Pia
mwiteni Hushai, Mwariki, ili tuweze
kusikia anachokisema.” 6 Hushai alipokuja,
Absalomu akasema, “Ahithofeli ametoa
shauri hili. Je, tufanye anavyosema? Kama
sivyo, tupe maoni yako.”
7 Hushai akamjibu Absalomu, “Shauri la
Ahithofeli alilotoa halifai kwa wakati huu.
8 [h]Unamfahamu baba yako na watu wake,
ni wapiganaji hodari, nao ni wakali kama
dubu mwitu aliyepokonywa watoto wake.
Zaidi ya hayo, baba yako ni mpiganaji jasiri,
usiku hatalala pamoja na vikosi. 9 [i]Hata
sasa, amefichwa ndani ya pango au mahali
pengine. Kama atatangulia kushambulia
vikosi vyako, yeyote asikiaye habari
hii atasema, ‘Kuna machinjo makubwa
miongoni mwa vikosi vinavyomfuata
Absalomu.’ 10 [j]Basi hata yule askari hodari
kuliko wengine wote, ambaye moyo wake
ni kama wa simba, atayeyuka kwa hofu,
kwa maana Israeli yote wanajua kwamba
baba yako ni mpiganaji na kwamba wale
walio pamoja naye ni watu hodari.
11 [k]“Kwa hiyo nakushauri: Israeli wote na
wakusanyikie kwako, kuanzia Dani hadi
Beer-Sheba, katika wingi wao jinsi walivyo
kama mchanga wa ufuoni mwa bahari,
wewe mwenyewe ukiwaongoza vitani.
12 Ndipo tutakapomshambulia popote
atakapoonekana, nasi tutamwangukia
kama umande unavyoshuka juu ya ardhi.
Yeye mwenyewe wala watu wake hakuna
atakayeachwa hai. 13 [l]Kama atakimbilia
katika mji wowote, basi Israeli wote
watazungushia mji ule kamba, nasi
tutauburuta mji huo mpaka bondeni hadi
isionekane hata changarawe ya huo mji.”
14 [m]Absalomu na watu wote wa Israeli
wakasema, “Shauri la Hushai, Mwariki,
ni jema zaidi kuliko lile la Ahithofeli.”
Kwa maana Bwana alikuwa amekusudia
kupinga shauri nzuri la Ahithofeli, ili kuleta
maafa juu ya Absalomu.
15 Hushai akawaambia makuhani Sadoki
na Abiathari, “Ahithofeli amemshauri
Absalomu na wazee wa Israeli kufanya

[a]**16:20** Kut 1:10; Za 37:12-15; Mit 21:30; Mt 27:1
[b]**16:21** Mwa 35:22; 2Sam 12:11; 15:16; Zek 8:13; Law 8:18; 20:11; Kum 22:30; 27:20; Mit 28:7; Isa 3:9; Mik 7:3-6
[c]**16:22** 2Sam 3:7; 12:11-12; 15:16
[d]**16:23** 2Sam 17:14, 23; 15:12
[e]**17:2** 2Sam 16:14; 1Fal 22:31; Zek 13:7; Kut 25:18; Yn 11:50; Mt 21:38
[f]**17:3** Yer 6:14
[g]**17:5** 2Sam 15:32
[h]**17:8** Hos 13:8; 1Sam 16:18; Amu 18:25
[i]**17:9** Yer 41:9
[j]**17:10** 1Nya 12:8; Yos 2:9-11; Eze 21:15; 2Sam 23:8; 1Nya 11:11
[k]**17:11** Amu 20:1; Mwa 12:2; Yos 11:4; Mwa 22:17
[l]**17:13** Mik 1:6
[m]**17:14** 2Sam 16:23; 15:12; 15:34; Neh 4:15; Za 9:16; 2Nya 10:8

kadha wa kadha, lakini mimi nimewashauri
wao kufanya kadha wa kadha. 16 [a]Sasa
tumeni ujumbe haraka na kumwambia
Daudi, ‘Usiku huu usilale kwenye vivuko
katika jangwa; vuka bila kukosa, la sivyo,
mfalme pamoja na watu wote waliofuatana
naye watamezwa.’ ”

17 [b]Yonathani na Ahimaasi walikuwa
wakingoja huko En-Rogeli, naye mtumishi
mmoja wa kike akawa anakwenda
kuwapasha habari nao wakawa
wanakwenda kumwambia Mfalme Daudi,
kwa maana wasingetaka kujihatarisha
kuonekana wakiingia mjini. 18 [c]Lakini
kijana mmoja mwanaume akawaona, naye
akamwambia Absalomu. Basi wote wawili
wakaondoka haraka, wakaenda mpaka
kwenye nyumba ya mtu mmoja huko
Bahurimu. Mtu huyo alikuwa na kisima
katika ua wa nyumba yake, nao Yonathani
na Ahimaasi wakateremka ndani ya kisima
hicho. 19 [d]Mkewe akachukua kifuniko,
akakiweka kwenye mdomo wa kile kisima
na kuanika nafaka juu yake. Hakuna mtu
yeyote aliyefahamu chochote kuhusu jambo
hilo.

20 [e]Watu wa Absalomu walipofika kwa
huyo mwanamke, wakamuuliza, “Wako
wapi Ahimaasi na Yonathani?”

Huyo mwanamke akawajibu, “Walivuka
kijito.” Watu wa Absalomu wakapekua
lakini hawakuwaona hata mmoja, hivyo
wakarudi Yerusalemu.

21 Baada ya watu hao kuondoka, wale
watu wawili yaani Yonathani na Ahimaasi
wakapanda kutoka mle kisimani na
kwenda kumpasha Mfalme Daudi habari.
Wakamwambia, “Ondoka, uvuke haya
maji haraka. Ahithofeli ameshauri kadha
wa kadha dhidi yako.” 22 Kwa hiyo Daudi
na watu wote aliokuwa nao waliondoka
na kuvuka Yordani. Kufika wakati wa
mapambazuko, hapakuwa na mtu hata
mmoja ambaye alikuwa hajavuka Mto
Yordani.

23 [f]Ahithofeli alipoona kwamba shauri
lake halikufuatwa, akatandika punda
wake, akaondoka kwenda nyumbani kwake
kwenye mji wake. Akaiweka nyumba
yake katika utaratibu, kisha akajinyonga
mwenyewe. Hivyo akafa na akazikwa
katika kaburi la baba yake.

24 [g]Daudi akaenda Mahanaimu, naye
Absalomu akavuka Yordani pamoja na
watu wote wa Israeli. 25 [h]Absalomu alikuwa
amemweka Amasa juu ya jeshi badala ya
Yoabu. Amasa alikuwa mwana wa mtu
mmoja aliyeitwa Yetheri, Mwisraeli,
ambaye alikuwa amemwoa Abigaili binti
Nahashi, dada yake Seruya mamaye Yoabu.
26 Waisraeli na Absalomu wakapiga kambi
huko nchi ya Gileadi.

27 [i]Daudi alipofika Mahanaimu, Shobi
mwana wa Nahashi kutoka Raba ya
Waamoni, Makiri mwana wa Amieli
kutoka Lo-Debari, na Barzilai Mgileadi
kutoka Rogelimu 28 [j]wakaleta matandiko
ya kitandani, mabakuli na vyombo vya
mfinyanzi. Walileta pia ngano na shayiri,
unga na bisi, maharagwe na kunde, 29 [k]asali
na maziwa yaliyoganda, kondoo na jibini
kutoka kwenye maziwa ya ng’ombe kwa
ajili ya Daudi na watu wake ili wale. Kwa
maana walisema, “Watu wameona njaa,
tena wamechoka na wamepata kiu huko
jangwani.”

*Kifo Cha Absalomu*

18 Daudi akakusanya watu aliokuwa nao
na kuweka majemadari wa maelfu na
majemadari wa mamia. 2 [l]Daudi akatuma

---

[a]**17:16** 2Sam 15:28-35
[b]**17:17** 2Sam 15:27, 36; Ay 15:7; 18:16; 1Fal 1:9; Yos 2:4; 15:7
[c]**17:18** 2Sam 3:16; 16:5
[d]**17:19** Yos 2:9
[e]**17:20** Kut 1:19; Yos 2:3-5; 1Sam 19:12-18; 21:2
[f]**17:23** 2Sam 16:23; 2Fal 20:1; 2Sam 15:12; Mt 27:5; Za 55:23; Ay 31:3
[g]**17:24** Mwa 32:2; 2Sam 2:8; Yos 13:26
[h]**17:25** 2Sam 19:13; 20:4-12; 1Fal 2:5, 32; 1Nya 12:18; 2:13-17
[i]**17:27** 1Sam 11:1; Kum 3:11; 2Sam 9:4; 19:31-39; 1Fal 2:7; Ezr 2:61; 2Sam 12:30
[j]**17:28** 1Sam 25:18; Mit 11:25; Mt 5:7
[k]**17:29** 1Nya 12:40; 2Sam 16:2; Rum 12:13; Kut 15:7; Amu 8:4-6; Za 34:8-10
[l]**18:2** Amu 7:16; 1Sam 11:11; 26:6; 2Sam 15:19

vikosi vya askari: theluthi moja ilikuwa
chini ya amri ya Yoabu, theluthi ya pili
chini ya Abishai mwana wa Seruya nduguye
Yoabu, na theluthi ya tatu chini ya Itai,
Mgiti. Mfalme akaviambia vikosi, "Hakika
mimi mwenyewe nitakwenda pamoja
nanyi."
3 [a]Lakini watu wakasema, "Haikupasi
kwenda, ikiwa sisi tutalazimika kukimbia,
wao hawatatujali. Hata kama nusu yetu
tukifa hawatajali, lakini wewe una thamani
ya watu kama sisi kumi elfu. Ingekuwa bora
zaidi kwako basi kutupatia msaada kutoka
mjini."
4 Mfalme akajibu, "Nitafanya lolote
linaloonekana jema zaidi kwenu."
Kwa hiyo mfalme akasimama kando ya
lango wakati watu wote wakitoka nje kwa
makundi ya mamia na maelfu. 5 Mfalme
akawaamuru Yoabu, Abishai na Itai,
"Kuweni wapole kwa kijana Absalomu kwa
ajili yangu." Vikosi vyote vikasikia mfalme
akitoa amri kwa kila jemadari kumhusu
Absalomu.
6 [b]Jeshi likatoka kwenda kwenye uwanja
wa vita kupigana na Israeli, hivyo vita
vikapiganwa katika msitu wa Efraimu.
7 [c]Huko jeshi la Israeli likashindwa na watu
wa Daudi, siku hiyo majeruhi walikuwa
wengi kiasi cha watu ishirini elfu. 8 Vita
vikaenea nchi nzima, watu wengi zaidi
wakifia msituni siku hiyo kuliko waliouawa
kwa upanga.
9 [d]Basi ikawa Absalomu alikutana na
watu wa Daudi. Yeye alikuwa amepanda
nyumbu wake, naye nyumbu alipopita
chini ya matawi yaliyosongana ya mwaloni
mkubwa, kichwa cha Absalomu kilinaswa
kwenye mti. Akaachwa akining'inia hewani,
wakati nyumbu aliyekuwa amempanda
aliendelea kwenda.
10 Mmojawapo wa wale watu alipoona,
akamwambia Yoabu, "Nimemwona
Absalomu akining'inia kwenye mti wa
mwaloni."

[a]**18:3** 1Sam 18:7; 2Sam 21:17
[b]**18:6** Yos 17:15-18
[c]**18:7** Mit 11:21
[d]**18:9** 2Sam 14:26; 17:23; Ay 18:5-14; Mt 27:5; 1Kor 11:14

11 [e]Yoabu akamwambia huyo mtu, "Nini!
Ulimwona Absalomu? Kwa nini hukumpiga
papo hapo mpaka chini? Ndipo ningekupa
shekeli kumi[f] za fedha na mkanda wa
askari shujaa."
12 Lakini huyo mtu akamjibu Yoabu,
"Hata kama ningepimiwa shekeli 1,000[g]
mikononi mwangu, nisingeinua mkono
wangu dhidi ya mwana wa mfalme. Tukiwa
tunasikia, mfalme alikuagiza wewe na
Abishai pamoja na Itai, akisema, 'Mlindeni
kijana Absalomu kwa ajili yangu.' 13 [h]Nami
kama ningekuwa nimemtendea kwa hila,
na hakuna lolote linalofichika kwa mfalme,
wewe mwenyewe ungejitenga nami."
14 [i]Yoabu akasema, "Mimi sitapoteza
muda hapa pamoja nawe." Hivyo
akachukua mikuki mitatu mkononi mwake,
akamchoma Absalomu nayo moyoni
alipokuwa angali hai akining'inia katika
ule mwaloni. 15 [j]Nao wabeba silaha kumi
wa Yoabu wakamzunguka Absalomu,
wakampiga na kumuua.
16 [k]Kisha Yoabu akapiga tarumbeta,
navyo vikosi vikaacha kuwafuata Israeli,
kwa maana Yoabu aliwasimamisha.
17 [l]Wakamchukua Absalomu, wakamtupa
katika shimo kubwa huko msituni na
kulundika lundo kubwa la mawe juu yake.
Huko nyuma, Waisraeli wote wakakimbilia
nyumbani kwao.
18 [m]Wakati wa uhai wa Absalomu alikuwa
amechukua nguzo na kuisimamisha katika
Bonde la Mfalme, kwa maana alifikiri, "Sina
mwana atakayeendeleza kumbukumbu ya
jina langu." Akaita nguzo hiyo kwa jina

[e]**18:11** 2Sam 3:39; 1Sam 18:4
[f]11 Shekeli kumi za fedha ni sawa na gramu 115.
[g]12 Shekeli 1,000 za fedha ni sawa na kilo 11.5.
[h]**18:13** 2Sam 14:19-20
[i]**18:14** 2Sam 2:18; 14:30
[j]**18:15** 2Sam 15:10
[k]**18:16** 2Sam 2:28; 20:22
[l]**18:17** Yos 7:26; 8:29; Yer 22:18, 19; Mao 3:53
[m]**18:18** Mwa 14:17; 50:5; Hes 32:42; 2Sam 14:27; 1Sam 15:12; Ay 13:12; 18:17-19; Za 34:16; 109:13; Mit 2:22

lake mwenyewe. Nayo inaitwa Mnara wa
Ukumbusho wa Absalomu mpaka leo.

*Daudi Aomboleza Kifo Cha Absalomu*

19 [a]Basi Ahimaasi mwana wa Sadoki
akasema, "Niruhusu mimi nikimbie na
kumpelekea mfalme habari kwamba BWANA
amemwokoa mfalme kutoka mikononi mwa
adui zake."
20 Yoabu akamwambia Ahimaasi, "Leo
si wewe utakayepeleka habari. Unaweza
kupeleka habari wakati mwingine, lakini
leo haikupasi kupeleka, kwa sababu mwana
wa mfalme amekufa."
21 Ndipo Yoabu akamwambia mtu mmoja
Mkushi, "Nenda, ukamwambie mfalme kile
ulichoona." Mkushi akasujudu mbele ya
Yoabu akaondoka mbio.
22 Ahimaasi mwana wa Sadoki
akamwambia tena Yoabu, "Liwalo na liwe,
tafadhali niruhusu nikimbie nyuma ya huyo
Mkushi."

Lakini Yoabu akajibu, "Mwanangu, mbona wataka kwenda? Wewe huna habari yoyote itakayokupa tuzo."
23 Ahimaasi akasema, "Liwalo na liwe,
nataka kukimbia."

Kwa hiyo Yoabu akamwambia, "Haya, kimbia!" Ndipo Ahimaasi akakimbia kufuata njia ya kupitia tambarare, akafika kabla ya huyo Mkushi.
24 [b]Wakati Daudi alipokuwa ameketi kati
ya lango la ndani na la nje, mlinzi akapanda
juu ya paa la lango kupitia ukutani.
Alipotazama nje, akaona mtu mmoja
akikimbia peke yake. 25 Mlinzi akampazia
mfalme sauti na kumpa taarifa.

Mfalme akasema, "Ikiwa yuko peke yake, lazima atakuwa na habari njema." Naye yule mtu akazidi kusogea karibu.
26 [c]Kisha mlinzi akaona mtu mwingine
anakuja akikimbia, akamwita bawabu,
"Tazama, mtu mwingine anakuja akikimbia
peke yake!"

Mfalme akasema, "Lazima atakuwa analeta habari njema pia."
27 [d]Mlinzi akasema, "Ninaona kuwa yule
wa kwanza anakimbia kama Ahimaasi
mwana wa Sadoki."

Mfalme akasema, "Yeye ni mtu mwema. Analeta habari njema."
28 Ndipo Ahimaasi akamwita mfalme,
akasema, "Mambo yote ni mema!"
Akasujudu mbele ya mfalme uso wake
mpaka ardhini, akasema, "Ahimidiwe
BWANA Mungu wako! Yeye aliyewatoa
watu wale walioinua mikono yao dhidi ya
mfalme bwana wangu."
29 Mfalme akauliza, "Je, huyo kijana
Absalomu yuko salama?"

Ahimaasi akajibu, "Kulikuwa na machafuko mengi mara tu Yoabu alipokuwa anataka kumtuma mtumishi wa mfalme pamoja nami mtumishi wako, lakini sijui ilikuwa nini?"
30 Mfalme akasema, "Simama kando na
usubiri hapa." Basi akasogea kando na
kusimama hapo.
31 [e]Ndipo huyo Mkushi akawasili na
kusema, "Mfalme bwana wangu, sikia
habari njema! Leo BWANA amekuokoa
kutoka kwa wale wote walioinuka dhidi
yako."
32 [f]Mfalme akamuuliza huyo Mkushi, "Je,
kijana Absalomu yuko salama?"

Huyo Mkushi akajibu, "Adui wa mfalme bwana wangu na wote wale walioinuka kukudhuru na wawe kama huyo kijana."
33 [g]Mfalme akatetemeka. Akapanda
chumbani juu kupitia langoni akilia.
Alipokuwa akienda, akasema, "Ee
mwanangu Absalomu! Mwanangu,
mwanangu Absalomu! Laiti ningekufa
badala yako: Ee Absalomu, mwanangu,
mwanangu!"

*Yoabu Amkemea Mfalme*

19 Yoabu akaambiwa, "Mfalme analia na
kumwombolezea Absalomu." 2 Kwa
jeshi lote, ushindi wa siku ile ukageuka
kuwa maombolezo, kwa sababu siku

[a]**18:19** 2Sam 15:36; Amu 11:36; 2Sam 17:17
[b]**18:24** 1Sam 14:16; Yer 51:12; 1Sam 4:13; 2Sam 13:34; 2Fal 9:17; Isa 21:6-9
[c]**18:26** 1Fal 1:42; Isa 52:7; 61:1
[d]**18:27** 2Fal 9:20
[e]**18:31** Za 27:3; 55:18
[f]**18:32** Amu 5:31; 1Sam 25:26
[g]**18:33** Kut 32:32; Mwa 43:14; 2Sam 19:4; Rum 9:3; Mit 10:1; 19:13

ile vikosi vilisikia ikisemwa, "Mfalme
anahuzunika kwa ajili ya mwanawe." 3 Siku
ile watu wakaingia mjini kimya kama vile
waingiavyo kwa aibu watu waliokimbia
kutoka vitani. 4 [a]Mfalme akafunika uso wake
akalia kwa sauti, akisema, "Ee mwanangu
Absalomu! Ee Absalomu, mwanangu,
mwanangu!"

5 Kisha Yoabu akaingia ndani ya nyumba
ya mfalme na kusema, "Leo umewaaibisha
watu wako wote, waliookoa maisha yako,
maisha ya wanao na binti zako, maisha ya
wake zako na masuria wako. 6 Unawapenda
wale wanaokuchukia, na unawachukia wale
wanaokupenda. Leo umeonyesha wazi
kwamba majemadari wako na watu wao
hawana maana kwako. Naona kwamba
ungefurahi kama Absalomu angekuwa hai
leo na sisi sote tuwe tumekufa. 7 [b]Sasa utoke
nje ukawatie moyo watu wako. Naapa
kwa BWANA kwamba ikiwa hutatoka nje,
hakuna mtu atakayesalia pamoja nawe
ifikapo leo jioni. Hii itakuwa mbaya zaidi
kwako kuliko maafa yote yaliyokupata
tangu ujana wako hadi sasa."

8 [c]Kwa hiyo mfalme akaondoka
akaketi kitini pake penye lango. Watu
walipoambiwa, "Mfalme ameketi langoni,"
watu wote wakamjia.

### *Daudi Arudi Yerusalemu*

Wakati huo, Waisraeli walikuwa
wamekimbilia nyumbani kwao. 9 [d]Katika
makabila yote ya Israeli, watu walikuwa
wanabishana wao kwa wao, wakisema,
"Mfalme alituokoa kutoka mikononi
mwa adui zetu; ndiye alituokoa kutoka
mikononi mwa Wafilisti. Lakini sasa
mfalme ameikimbia nchi kwa sababu ya
Absalomu, 10 naye Absalomu, tuliyemtia
mafuta atutawale, amekufa vitani. Basi
mbona hamsemi lolote kuhusu kumrudisha
mfalme?"

11 [e]Mfalme Daudi akapeleka ujumbe
huu kwa makuhani Sadoki na Abiathari,
kusema: "Waulizeni wazee wa Yuda, 'Kwa
nini mwe wa mwisho kumrudisha mfalme
katika jumba lake la kifalme, maadamu
kile kinachosemwa katika Israeli yote
kimemfikia mfalme katika makao yake?
12 [f]Ninyi ni ndugu zangu, nyama yangu na
damu yangu mwenyewe. Kwa hiyo kwa
nini mwe wa mwisho kumrudisha mfalme?'
13 [g]Nanyi mwambieni Amasa, 'Je, wewe si
nyama yangu mwenyewe na damu yangu?
Mungu na anishughulikie, tena kwa ukali,
kama kuanzia sasa na kuendelea wewe si
jemadari wa jeshi langu mahali pa Yoabu.' "

14 [h]Aliipata mioyo ya watu wote wa
Yuda kama vile walikuwa mtu mmoja.
Wakapeleka ujumbe kwa mfalme, kusema,
"Rudi, wewe na watu wako wote." 15 [i]Ndipo
mfalme akarudi, akaenda hadi kufikia Mto
Yordani.

Basi watu wa Yuda walikuwa wamekuja
mpaka Gilgali ili kutoka kwenda kumlaki
mfalme na kumvusha Mto Yordani.
16 [j]Shimei mwana wa Gera, wa kabila la
Benyamini kutoka Bahurimu, akaharakisha
kuteremka pamoja na watu wa Yuda ili
kumlaki Mfalme Daudi. 17 [k]Pamoja naye
walikuwepo Wabenyamini elfu moja
wakiwa wamefuatana na Siba, msimamizi
wa nyumba ya Sauli, pia wanawe kumi
na watano, na watumishi ishirini.
Wakaharakisha kwenda Yordani, mahali
mfalme alipokuwa. 18 Wakavuka kivuko
ili kuwachukua watu wa nyumbani mwa
mfalme ili kuwavusha na kufanya kila kitu
alichotaka.

Shimei mwana wa Gera alipovuka
Yordani, akaanguka kifudifudi mbele

---

[a]**19:4** 2Sam 15:30; 18:33; 1Sam 4:12
[b]**19:7** Mit 14:28
[c]**19:8** 2Sam 15:2; Rut 4:1; 2Sam 18:4, 24; 2Fal 14:12; 1Fal 12:16
[d]**19:9** 2Sam 8:1-14; 15:14; 5:18; 1Sam 17:1; 18:1
[e]**19:11** 2Sam 15:24
[f]**19:12** Mwa 2:23; Amu 9:2; 2Sam 5:1
[g]**19:13** 2Sam 17:25; Mwa 29:14; Rut 1:17; 2Sam 2:13; 1Fal 8:16; 1Nya 2:16; 17:12, 18; 1Fal 19:2
[h]**19:14** Amu 20:1; Za 110:2-3; Mdo 4:32
[i]**19:15** 1Sam 11:15; Yos 5:9
[j]**19:16** 2Sam 16:5-13; 1Fal 2:8
[k]**19:17** 2Sam 9:2; Mwa 43:16; 2Sam 16:1-2

ya mfalme, [19] [a]na kumwambia, “Bwana
wangu na asinihesabie hatia. Usikumbuke
jinsi mtumishi wako alivyofanya kosa siku
ile bwana wangu mfalme alipoondoka
Yerusalemu. Mfalme aliondoe moyoni
mwake. [20] [b]Kwa maana mimi mtumishi
wako najua nimefanya dhambi, lakini
leo nimekuja hapa kama wa kwanza wa
nyumba yote ya Yosefu kushuka na kumlaki
bwana wangu mfalme.”

[21] [c]Ndipo Abishai mwana wa Seruya
akasema, “Je, Shimei hapaswi kuuawa kwa
ajili ya hili? Alimlaani mpakwa mafuta wa
Bwana.”

[22] [d]Daudi akajibu, “Mimi nina nini nanyi,
enyi wana wa Seruya? Leo hii mmekuwa
adui zangu! Je, leo kuna yeyote atakayeuawa
katika Israeli? Je, mimi sijui kuwa leo ndimi
mfalme katika Israeli yote?” [23] [e]Basi mfalme
akamwambia Shimei, “Hutakufa.” Naye
mfalme akamwahidi kwa kiapo.

[24] [f]Pia Mefiboshethi mwana wa Sauli
akashuka kwenda kumlaki mfalme. Hakuwa
amenawa miguu wala kunyoa ndevu zake
wala kufua nguo zake tangu siku mfalme
alipoondoka Yerusalemu mpaka siku
aliporudi ile salama. [25] [g]Wakati alipotoka
Yerusalemu kuja kumlaki mfalme, mfalme
akamuuliza, “Mefiboshethi, kwa nini
hukufuatana nami?”

[26] [h]Akasema, “Bwana wangu mfalme,
maadamu mimi mtumishi wako ni kiwete,
nilisema, ‘Nitandikiwe punda wangu,
nimpande, ili niweze kwenda pamoja na
mfalme.’ Lakini Siba mtumishi wangu
akanisaliti. [27] [i]Naye amemchongea mtumishi
wako kwa bwana wangu mfalme. Bwana
wangu mfalme ni kama malaika wa Mungu,
kwa hiyo fanya lolote linalokupendeza.
[28] [j]Wazao wote wa baba yangu hawastahili
kitu kingine isipokuwa kifo kutoka kwa
bwana wangu mfalme, lakini ulimpa
mtumishi wako nafasi miongoni mwa wale
waliokula mezani pako. Je, ninayo haki
gani kumwomba mfalme zaidi ya hayo?”

[29] [k]Mfalme akamwambia, “Kwa nini
useme zaidi? Naamuru wewe na Siba
mgawanye mashamba.”

[30] Mefiboshethi akamwambia mfalme,
“Mruhusu achukue kila kitu, kwa kuwa sasa
bwana wangu mfalme amerudi nyumbani
salama.”

[31] [l]Barzilai, Mgileadi, pia akashuka
kutoka Rogelimu ili kuvuka Yordani pamoja
na mfalme na kumsindikiza kutoka huko.
[32] [m]Basi Barzilai alikuwa mzee sana mwenye
umri wa miaka themanini. Alikuwa
amempatia mfalme mahitaji wakati
alipokuwa anaishi huko Mahanaimu, kwa
kuwa alikuwa mtu tajiri sana. [33] Mfalme
akamwambia Barzilai, “Vuka pamoja nami
na ukae nami huko Yerusalemu, nami
nitakupatia mahitaji yako.”

[34] [n]Lakini Barzilai akamjibu mfalme,
“Je, nitaishi miaka mingine mingapi, hata
nipande kwenda Yerusalemu pamoja na
mfalme? [35] [o]Sasa nina miaka themanini.
Je, naweza kutofautisha kati ya lililo
jema na lililo baya? Je, mtumishi wako
anaweza kujua ladha ya kile anachokula
au anachokunywa? Je, bado naweza
kusikiliza sauti za waimbaji wa kiume na
za wanawake? Kwa nini mtumishi wako
aongeze mzigo kwa bwana wangu mfalme?
[36] Mtumishi wako atavuka Yordani pamoja
na mfalme kwa umbali mfupi tu, lakini kwa
nini mfalme anizawadie kwa namna hii?

---

[a]**19:19** 2Sam 16:6-8; 1Sam 22:13; Za 32:2; Rum 4:6-8; 2Kor 5:19; Mit 28:13; Mt 5:25; 2Sam 16:5-6; 13:33
[b]**19:20** 2Sam 16:5
[c]**19:21** 1Sam 26:6; Kut 22:28; 1Sam 12:3; 26:9; 2Sam 16:7-8; Mhu 10:20; Mdo 23:5; 2Pet 2:10-11; Yud 8
[d]**19:22** 2Sam 2:18; 16:10; 1Sam 11:13; 16:8; Mt 8:29
[e]**19:23** 1Fal 2:8, 42
[f]**19:24** 2Sam 4:4; 9:6-10
[g]**19:25** 2Sam 16:17
[h]**19:26** Law 21:18; 2Sam 9:2
[i]**19:27** 1Sam 29:9; 2Sam 14:17-20; 16:3; Za 15:3; 63:11; Mit 21:6; 26:28; Yer 9:4-5
[j]**19:28** 1Sam 25:2; 2Sam 17:27; 9:7-13
[k]**19:29** Kum 19:16-21; Za 82:2; 101:1-8; Mit 29:4
[l]**19:31** Za 90:10; 2Nya 35:25; Ezr 2:65; Mhu 2:8; 12:1; 2Sam 15:33; 1Fal 2:7; Neh 7:63
[m]**19:32** 2Sam 17:27
[n]**19:34** Mwa 47:9; Za 39:4-5; Yak 4:14
[o]**19:35** Mwa 49:29; Yer 41:17; 1Fal 2:7; Za 90:10; Mhu 12:3-6

37 [a]Mruhusu mtumishi wako arudi, ili mimi
nikafie katika mji wangu mwenyewe karibu
na kaburi la baba yangu na mama yangu.
Lakini yupo hapa mtumishi wako Kimhamu.
Mruhusu avuke pamoja na bwana wangu
mfalme. Mtendee lolote linalokupendeza."
38 Mfalme akamwambia Barzilai,
"Kimhamu atavuka Yordani pamoja nami,
nami nitamtendea lolote litakalokupendeza.
Nawe kitu chochote unachotaka kutoka
kwangu nitakutendea."
39 [b]Kwa hiyo watu wote wakavuka
Yordani, kisha mfalme akavuka. Mfalme
akambusu Barzilai na kumbariki; Barzilai
akarudi nyumbani kwake.
40 Mfalme alipovuka kwenda Gilgali,
Kimhamu akavuka pamoja naye. Vikosi
vyote vya Yuda na nusu ya vikosi vya Israeli
vilimvusha mfalme.
41 [c]Baada ya kitambo kidogo watu
wote wa Israeli wakaja kwa mfalme na
kumwambia, "Kwa nini ndugu zetu, watu
wa Yuda, wamemrudisha mfalme kwa siri
bila kutushirikisha, na kumvusha ng'ambo
ya Yordani, yeye na nyumba yake, pamoja
na watu wake wote?"
42 [d]Watu wote wa Yuda wakawajibu watu
wa Israeli, "Tulifanya hivi kwa sababu
mfalme ni jamaa yetu wa karibu. Kwa nini
mnakasirikia jambo hili? Je, tumekula kitu
chochote cha mfalme? Je, tumejichukulia
kitu chochote kwa ajili yetu wenyewe?"
43 [e]Ndipo watu wa Israeli wakawajibu
watu wa Yuda, "Tunayo haki mara kumi
kwa mfalme; sisi tunahusika zaidi na Daudi
kuliko ninyi. Kwa nini basi mnatudharau?
Je, hatukuwa wa kwanza kuzungumza
kuhusu kumrudisha mfalme nyumbani?"

Lakini watu wa Yuda wakajibu kwa ukali hata zaidi kuliko watu wa Israeli.

[a]**19:37** Mwa 49:29; Yer 41:17; 1Fal 2:7
[b]**19:39** Mwa 47:7; 31:55; 14:19; Kut 39:43; Yos 22:6; 1Sam 2:20
[c]**19:41** Amu 8:1; 12:1; 2Sam 19:15
[d]**19:42** 2Sam 19:12; Rut 4:12; 1Nya 2:3-15; Za 78:68-70
[e]**19:43** 2Sam 5:1; 1Fal 11:30-31

### *Sheba Aasi Dhidi Ya Daudi*

20 [f]Basi, kulikuwa na mtu mbaya sana aliyeitwa Sheba mwana wa Bikri, Mbenyamini, aliyekuwako huko. Akapiga tarumbeta na kupaza sauti,

"Hatuna fungu katika Daudi,
  wala hatuna sehemu
  katika mwana wa Yese!
Kila mtu aende hemani mwake,
  enyi Israeli!"

2 [g]Kwa hiyo watu wote wa Israeli
wakamwacha Daudi na kumfuata Sheba
mwana Bikri. Lakini watu wa Yuda wakawa
karibu na mfalme wao katika safari yote
kutoka Yordani mpaka Yerusalemu.
3 [h]Daudi aliporudi katika jumba lake la
kifalme huko Yerusalemu, aliwachukua
wale masuria kumi aliokuwa amewaacha
ili kuangalia jumba la kifalme na kuwaweka
ndani ya nyumba chini ya ulinzi. Akawapa
mahitaji yao lakini hakukutana nao
kimwili. Waliwekwa kifungoni wakaishi
kama wajane mpaka kifo chao.
4 [i]Ndipo mfalme akamwambia Amasa,
"Waite watu wa Yuda waje kwangu katika
muda wa siku tatu, nawe mwenyewe uwepo
hapa." 5 Lakini Amasa alipokwenda kuwaita
Yuda, alichukua muda mrefu zaidi ya ule
mfalme aliokuwa amemwekea.
6 [j]Daudi akamwambia Abishai, "Sasa
Sheba mwana wa Bikri atatuletea madhara
zaidi kuliko alivyofanya Absalomu.
Wachukue watu wa bwana wako na
umfuatie, la sivyo atapata mji wenye ngome
na kututoroka." 7 [k]Hivyo watu wa Yoabu,
na Wakerethi na Wapelethi, pamoja na
wapiganaji mashujaa wote wakaondoka
chini ya uongozi wa Abishai. Wakatoka

[f]**20:1** Mwa 31:14; 29:14; 1Fal 12:16; 1Sam 22:7-8; 2Nya 10:16; 2Sam 12:10; Kum 13:13; Amu 19:22; 1Sam 2:12; 10:27; 1Fal 21:10-13; 2Nya 13:7; 2Sam 19:43
[g]**20:2** Mit 17:14
[h]**20:3** 2Sam 15:16; 16:21-22
[i]**20:4** 2Sam 17:25; 19:13
[j]**20:6** 2Sam 21:17; 1Sam 26:6; 2Sam 18:2; 11:11; 1Fal 1:33
[k]**20:7** 1Sam 30:14; 2Sam 15:18; 1Fal 1:38; 2Sam 8:18

Yerusalemu ili kumfuata Sheba mwana
wa Bikri.
8 [a]Wakati walikuwa kwenye mwamba
mkubwa huko Gibeoni, Amasa alikuja
kuwalaki. Yoabu alikuwa amevaa mavazi
yake ya kijeshi; juu yake alifunga mkanda
kwenye kiuno wenye upanga ndani ya ala.
Alipokuwa akienda mbele, ule upanga
ukaanguka kutoka kwenye ala.
9 [b]Yoabu akamwambia Amasa, "U
hali gani, ndugu yangu?" Kisha Yoabu
akamshika Amasa ndevu kwa mkono wake
wa kuume ili ambusu. 10 [c]Amasa hakuona
upanga uliokuwa mkononi mwa Yoabu,
naye Yoabu akamchoma nao tumboni, nayo
matumbo yake yakamwagika chini. Pasipo
kuchomwa mara ya pili, Amasa akafa. Basi
Yoabu na Abishai nduguye wakamfuatia
Sheba mwana wa Bikri.
11 Mmoja wa watu wa Yoabu akasimama
kando ya Amasa, akasema, "Yeyote
ampendaye Yoabu na yeyote aliye upande
wa Daudi, na amfuate Yoabu!" 12 [d]Amasa
alikuwa akigaagaa katika damu yake
katikati ya barabara; mtu mmoja akaona
kwamba vikosi vyote vilikuwa vinasimama
pale. Huyo mtu alipotambua kwamba kila
aliyefika pale Amasa alipokuwa alisimama,
alimburuta Amasa kutoka barabarani
mpaka kwenye shamba na kutupia nguo
juu yake. 13 Baada ya Amasa kuondolewa
kutoka barabarani, watu wote walienda
pamoja na Yoabu kumfuatia Sheba mwana
wa Bikri.
14 [e]Sheba akapita katika makabila yote ya
Israeli hadi Abel-Beth-Maaka na kupitia eneo
lote la Waberi ambao walijikusanya pamoja
na kumfuata. 15 [f]Vikosi vyote vya Yoabu
vikaja na kumhusuru Sheba mwana wa
Bikri huko Abel-Beth-Maaka. Wakauzingira
mji kwa kuweka vikosi vya askari, ili
kukabiliana na ngome ya mji. Walipokuwa
wanagongagonga ukuta ili kuubomoa na
kuuangusha chini, 16 [g]mwanamke mmoja
mwenye busara akaita kutoka ndani ya mji,
akisema, "Sikilizeni! Sikilizeni! Mwambieni
Yoabu aje hapa ili niweze kuzungumza
naye." 17 Yoabu alikwenda mbele yake,
akamuuliza, "Wewe ni Yoabu?"
Akamjibu, "Ndiye mimi."
Yule mwanamke akamwambia, "Sikiliza
kile mtumishi wako atakachokuambia."
Akamwambia, "Ninasikiliza."
18 Huyo mwanamke akaendelea kusema,
"Zamani za kale walikuwa wakisema,
'Wakaulize ushauri huko Abeli,' hivyo
kulimaliza lile shauri. 19 [h]Sisi ni watu wa
amani na waaminifu katika Israeli. Wewe
unajaribu kuharibu mji ambao ni mama
katika Israeli. Kwa nini unataka kumeza
urithi wa BWANA?"
20 Yoabu akajibu, "Hilo liwe mbali nami.
Hilo liwe mbali nami kumeza au kuharibu.
21 [i]Hivyo sivyo ilivyo. Mtu mmoja jina
lake Sheba mwana wa Bikri, kutoka nchi
ya vilima vya Efraimu, ameinua mkono
wake dhidi ya mfalme, dhidi ya Daudi.
Nikabidhini mtu huyu mmoja, nami
nitajiondoa katika mji huu."
Huyu mwanamke akamwambia Yoabu,
"Kichwa chake mtatupiwa kupitia juu ya
ukuta."
22 [j]Ndipo huyo mwanamke akaenda
kwa watu wote akiwa na ushauri wake wa
busara, nao wakakata kichwa cha Sheba
mwana wa Bikri na kumtupia Yoabu.
Kwa hiyo Yoabu akapiga tarumbeta, na
watu wake wakatawanyika kutoka mjini,
kila mmoja akirejea nyumbani kwake.
Naye Yoabu akarudi kwa mfalme huko
Yerusalemu.
23 [k]Yoabu alikuwa jemadari wa jeshi
lote la Israeli; Benaya mwana wa
Yehoyada alikuwa juu ya Wakerethi na

---

[a]**20:8** Yos 9:3; 2Sam 2:18
[b]**20:9** Mt 26:49; Lk 22:47; Mwa 4:8; 2Sam 2:23; 3:27; 1Fal 2:5
[c]**20:10** Amu 3:21; 2Sam 3:27; 1Fal 2:5
[d]**20:12** 2Sam 2:23
[e]**20:14** Hes 21:16; 1Fal 15:20; 2Fal 15:29; 2Nya 16:4
[f]**20:15** 1Fal 15:20; 2Fal 15:29; Isa 37:33; Yer 6:6; 32:24; Lk 19:43
[g]**20:16** 2Sam 14:2
[h]**20:19** Kum 2:26; 1Sam 26:19; 2Sam 21:3
[i]**20:21** 2Sam 4:8
[j]**20:22** Mhu 9:13-14; 7:19
[k]**20:23** 2Sam 2:28; 8:16-18; 24:2

Wapelethi; 24 [a]Adoramu alikuwa kiongozi
wa wale waliofanya kazi ya kulazimishwa;
Yehoshafati mwana wa Ahiludi alikuwa
mweka kumbukumbu; 25 [b]Sheva[c] alikuwa
mwandishi; Sadoki na Abiathari walikuwa
makuhani; 26 [d]na Ira, Myairi, alikuwa kuhani
wa Daudi.

*Wagibeoni Walipiza Kisasi*

21 [e]Wakati wa utawala wa Daudi kulikuwa
na njaa kwa miaka mitatu mfululizo,
kwa hiyo Daudi akautafuta uso wa BWANA.
BWANA akasema, "Ni kwa sababu ya Sauli
na nyumba yake iliyotiwa madoa ya damu,
kwa sababu aliwaua Wagibeoni."
2 [f]Mfalme akawaita Wagibeoni na
kuzumgumza nao. (Wagibeoni hawakuwa
wa wana wa Israeli, ila walikuwa mabaki
ya Waamori. Waisraeli walikuwa wameapa
kuwaacha hai, lakini Sauli katika wivu
wake kwa ajili ya Israeli na Yuda, alikuwa
amejaribu kuwaangamiza.) 3 [g]Daudi
akawauliza Wagibeoni, "Niwatendee
nini? Nitawaridhishaje ili mbariki urithi
wa BWANA?"
4 [h]Wagibeoni wakamjibu, "Hatuna haki
ya kudai fedha wala dhahabu kutoka kwa
Sauli au jamaa yake, wala hatuna haki ya
kumuua mtu yeyote katika Israeli."
Daudi akawauliza, "Mnataka niwafanyie
nini?"
5 Wakamjibu mfalme, "Kwa habari ya
mtu aliyetuangamiza na kufanya hila
mbaya dhidi yetu ili kwamba tuangamizwe
na tusiwe na yeyote katika Israeli,
6 [i]tupatieni wazao wake saba wa kiume
tuwaue hadharani mbele za BWANA huko
Gibea ya Sauli, aliyekuwa amechaguliwa
na BWANA."
Basi mfalme akasema, "Nitawakabidhi
kwenu."
7 [j]Mfalme akamhifadhi Mefiboshethi
mwana wa Yonathani, mwana wa Sauli, kwa
sababu ya kile kiapo mbele za BWANA kati
ya Daudi na Yonathani. 8 [k]Lakini mfalme
akamchukua Armoni na Mefiboshethi, wana
wawili wa Rispa binti Aiya, ambao alikuwa
amemzalia Sauli, pamoja na wana watano
wa Merabu binti Sauli, aliokuwa amemzalia
Adrieli mwana wa Barzilai, Mmeholathi.
9 [l]Akawakabidhi kwa Wagibeoni, ambao
waliwaua na kuwaweka wazi juu ya kilima
mbele za BWANA. Wote saba walianguka
kwa pamoja; waliuawa katika siku za
kwanza za mavuno, mara tu uvunaji wa
shayiri ulipokuwa unaanza.
10 [m]Rispa binti Aiya akachukua nguo
ya gunia, akajitandikia juu ya mwamba.
Kuanzia mwanzo wa mavuno mpaka
mvua ziliponyesha juu ya miili ya hao
waliouawa, Rispa hakuruhusu ndege wa
angani kuwagusa wakati wa mchana, wala
wanyama wa mwitu wakati wa usiku.
11 Daudi alipoambiwa kile Rispa binti Aiya,
suria wa Sauli, alichokuwa amekifanya,
12 [n]alikwenda akachukua mifupa ya Sauli
na mwanawe Yonathani kutoka kwa
watu wa Yabeshi-Gileadi. (Walikuwa
wameichukua kwa siri kutoka uwanja wa
watu wote huko Beth-Shani, mahali ambapo
Wafilisti walikuwa wamewatundika baada
ya kumuua Sauli huko Gilboa.) 13 Daudi
akaileta mifupa ya Sauli na ya mwanawe
Yonathani kutoka huko, pia mifupa ya
wale waliokuwa wameuawa na kutupwa
ilikusanywa.
14 [o]Wakazika mifupa ya Sauli na ya

---

[a]**20:24** 1Fal 4:6; 5:14; 12:18; 2Nya 10:18; 2Sam 8:16; 1Fal 4:3
[b]**20:25** 1Sam 2:35; 2Sam 8:17
[c]25 Sheva mahali pengine ameitwa Shausha (1Nya 18:16; 1Fal 4:3).
[d]**20:26** 2Sam 23:38
[e]**21:1** Mwa 12:10; Kum 32:24; Kut 32:11; Hes 27:21; 1Sam 22:10-15; Law 18:25; Hes 35:33; Isa 26:21
[f]**21:2** Yos 9:15; 9:3
[g]**21:3** 1Sam 26:19; 2Sam 20:19
[h]**21:4** Hes 35:33-34
[i]**21:6** Hes 25:4; 1Sam 10:24; Amu 20:4
[j]**21:7** 2Sam 4:4; 1Sam 18:3; 2Sam 9:7; 1Sam 20:8, 15
[k]**21:8** 2Sam 3:7; 1Sam 18:19
[l]**21:9** 2Sam 16:8; Rut 1:22; 2Sam 6:17
[m]**21:10** Mwa 40:19; 1Sam 17:44; Kum 21:23; 2Sam 3:7
[n]**21:12** 1Sam 31:11-13; Amu 21:8; 1Sam 11:1; Yos 17:11; 17:11; 1Sam 31:10; 28:4
[o]**21:14** Yos 18:28; 7:26; 2Sam 24:25; 1Nya 8:34

mwanawe Yonathani katika kaburi la Kishi,
babaye Sauli, huko Sela katika nchi ya
Benyamini, nao wakafanya kila kitu mfalme
alichoagiza. Baada ya hayo, Mungu akajibu
maombi kwa ajili ya nchi.

*Vita Dhidi Ya Wafilisti*

**(1 Nyakati 20:4-8)**

15 Kwa mara nyingine tena kulikuwa
na vita kati ya Wafilisti na Israeli. Daudi
akashuka pamoja na watu wake ili kupigana
dhidi ya Wafilisti, naye akawa amechoka
sana. 16 Naye Ishbi-Benobu, mmoja wa
wazao wa Warefai,[a] ambaye mkuki wake
ulikuwa na uzito wa shekeli 300 za shaba,[b]
alikuwa amejifunga upanga mpya, naye
alisema angemuua Daudi. 17 [c]Lakini Abishai
mwana wa Seruya akaja kumwokoa Daudi;
akampiga huyo Mfilisti, akamwangusha
chini na kumuua. Ndipo watu wakamwapia
Daudi, wakisema, “Kamwe hutakwenda
tena nasi vitani, ili kwamba taa ya Israeli
isije ikazimwa.”

18 [d]Baada ya muda, kukawa na vita
nyingine na Wafilisti, huko Gobu. Wakati
huo Sibekai, Mhushathi, akamuua Safu,
mmoja wa wazao wa Warefai.

19 [e]Katika vita vingine na Wafilisti huko
Gobu, Elhanani mwana wa Yaare-Oregimu,
Mbethlehemu, alimuua nduguye Goliathi,
Mgiti, ambaye mkuki wake ulikuwa na
mpini kama mti wa mfumaji.

20 [f]Katika vita vingine tena, vilivyopiganwa
huko Gathi, kulikuwako na mtu mmoja
mkubwa mwenye vidole sita katika kila
mkono na vidole sita kila mguu, jumla
vidole ishirini na vinne. Yeye alikuwa pia
mzao wa Mrefai. 21 [g]Alipowadhihaki Israeli,
Yonathani mwana wa Shimea, nduguye
Daudi, akamuua.

22 Hawa wanne walikuwa wazao wa
Warefai huko Gathi, nao walianguka kwa
mikono ya Daudi na watu wake.

*Wimbo Wa Daudi Wa Sifa*

**(Zaburi 18)**

22 [h]Daudi alimwimbia Bwana maneno
ya wimbo huu wakati Bwana
alipomwokoa mikononi mwa adui
zake wote, na pia mkononi mwa Sauli.
2 [i]Akasema:

“Bwana ni mwamba wangu,
ngome yangu na mwokozi wangu,
3 [j]Mungu wangu ni mwamba wangu,
ambaye kwake ninakimbilia,
ngao yangu na pembe ya wokovu
wangu.
Yeye ni ngome yangu, kimbilio
langu
na mwokozi wangu,
huniokoa kutoka kwa watu wenye
jeuri.
4 [k]Ninamwita Bwana, anayestahili
kusifiwa,
nami ninaokolewa kutoka kwa
adui zangu.

5 [l]“Mawimbi ya mauti yalinizunguka,
mafuriko ya maangamizi
yalinilemea.
6 [m]Kamba za kuzimu[n] zilinizunguka,
mitego ya mauti ilinikabili.
7 [o]Katika shida yangu nalimwita
Bwana,
nilimlilia Mungu wangu.

---

[a]16 Yaani majitu.
[b]16 Shekeli 300 za shaba ni sawa na kilo 3.5.
[c]**21:17** 2Sam 20:6; 1Fal 11:36; 15:4; 2Fal 8:19; 2Nya 21:7; Za 132:17; 2Sam 18:3
[d]**21:18** 1Nya 11:29; 27:11
[e]**21:19** 1Sam 17:4-7
[f]**21:20** 1Nya 20:6
[g]**21:21** 1Sam 17:10; 16:9
[h]**22:1** Kut 15:1; Amu 5:1; Za 18:2-50
[i]**22:2** 1Sam 2:2; Za 31:3; 91:2; 71:3; 144:2; Kum 32:4; Za 18:2; Mit 18:10; Mt 18:10
[j]**22:3** Mit 10:29; Yoe 3:16; Kum 23:15; 32:37; Za 14:6; 31:2; 59:16; 71:7; 91:2; 94:22; Isa 25:4; Yer 16:19; Mwa 15:1; Kum 33:17; Lk 1:69; Za 9:9; 52:7
[k]**22:4** Za 48:1; 96:4; 145:3
[l]**22:5** Za 69:14-15; Yon 2:3
[m]**22:6** Za 116:3; Mdo 2:24
[n]6 Kuzimu kwa Kiebrania ni Sheol, maana yake ni Shimo lisilo na mwisho.
[o]**22:7** Mwa 35:3; Amu 2:15; 2Nya 15:4; Za 4:1; 77:2; 120:1; Isa 26:16; Za 34:15; 116:4; 116:4; Kut 3:7

Kutoka Hekaluni mwake alisikia
sauti yangu,
kilio changu kikafika masikioni
mwake.

8 [a]"Dunia ilitetemeka na kutikisika,
misingi ya mbingu ikatikisika,
vilitetemeka kwa sababu
alikuwa amekasirika.
9 [b]Moshi ukapanda kutoka puani
mwake,
moto uteketezao ukatoka kinywani
mwake,
makaa ya moto yawakayo
yakatoka ndani mwake.
10 [c]Akazipasua mbingu akashuka chini,
mawingu meusi yalikuwa chini ya
miguu yake.
11 [d]Alipanda juu ya kerubi akaruka,
akapaa juu kwa mbawa za upepo.
12 [e]Alifanya giza hema lake la
kujifunika:
mawingu meusi ya mvua ya
angani.
13 [f]Kutokana na mwanga wa uwepo
wake
mawingu yalisogea,
ikanyesha mvua ya mawe
na umeme wa radi.
14 [g]BWANA alinguruma kutoka
mbinguni,
sauti ya Aliye Juu Sana ilisikika.
15 [h]Aliipiga mishale na kutawanya adui,
umeme wa radi na kuwafukuza.
16 [i]Mabonde ya bahari yalifunuliwa,
na misingi ya dunia ikawa wazi
kwa kukaripia kwake BWANA,
kwa uvumi wa pumzi kutoka
puani mwake.

17 [j]"Alinyoosha mkono kutoka juu na
kunishika;
alinitoa kutoka kilindi cha maji
makuu.
18 [k]Aliniokoa kutoka adui wangu
mwenye nguvu nyingi,
kutoka adui zangu waliokuwa na
nguvu nyingi kuliko mimi.
19 [l]Walinikabili siku ya msiba wangu,
lakini BWANA alikuwa msaada
wangu.
20 [m]Alinileta nje mahali penye nafasi
tele,
akaniokoa kwa kuwa alipendezwa
nami.

21 [n]"BWANA alinitendea sawasawa na
uadilifu wangu;
sawasawa na usafi wa mikono
yangu amenilipa.
22 [o]Kwa maana nimezishika njia za
BWANA;
sijatenda ubaya nikamwacha
Mungu wangu.
23 [p]Sheria zake zote zi mbele yangu,
wala sijayaacha maagizo yake.
24 [q]Nimekuwa sina hatia mbele zake,
nami nimejilinda nisitende
dhambi.
25 [r]BWANA amenilipa sawasawa na
uadilifu wangu,
sawasawa na usafi wangu machoni
pake.

---

[a]**22:8** Amu 5:4; Za 97:4; Kut 19:18; Za 68:8; 77:18; Yer 10:10; Ay 9:6; 26:11; Za 75:3
[b]**22:9** Za 50:3; 97:3; Ebr 12:29; Ufu 11:5; Isa 6:6; Eze 1:13; 10:2; Hab 3:5
[c]**22:10** Kut 19:9; Law 16:2; Kum 33:26; 1Fal 8:12; Ay 26:9; Za 104:3; Isa 19:1; Yer 4:13; Nah 1:3; Isa 64:1
[d]**22:11** Mwa 3:24; Kut 25:22; Za 104:3
[e]**22:12** Kut 19:9
[f]**22:13** Ay 37:3; Za 77:18
[g]**22:14** 1Sam 2:10; Isa 30:30
[h]**22:15** Kum 32:23; Za 7:13; 77:7; Hab 3:11
[i]**22:16** Za 6:1; 50:8, 21; 106:9; Nah 1:4; Isa 30:33; 40:24; Kut 14:21
[j]**22:17** Za 144:7; Kut 2; 10
[k]**22:18** Lk 1:71
[l]**22:19** Za 23:4
[m]**22:20** Ay 36:16; Za 31:8; 118:5; 22:8; Isa 42:1; Mt 12:18; 2Sam 15:26
[n]**22:21** 1Sam 26:23; Za 26:6; Ay 17:9; 22:30; 42:7-8; Za 24:4
[o]**22:22** Mwa 18:19; Za 128:1; Mit 8:32
[p]**22:23** Kum 6:4-9; Za 119:30-32, 102; Kum 7:12
[q]**22:24** Mwa 6:9; Efe 1:4; Yn 1:47
[r]**22:25** 1Sam 26:23

26 [a]"Kwa yeye aliye mwaminifu
unajionyesha kuwa
mwaminifu,
kwa asiye na hatia unajionyesha
kutokuwa na hatia,
27 [bc]kwa aliye mtakatifu unajionyesha
kuwa mtakatifu,
lakini kwa aliyepotoka
unajionyesha kuwa mkaidi.
28 [d]Wewe huwaokoa wanyenyekevu,
lakini macho yako ni juu ya wenye
kiburi
ili uwashushe.
29 [e]Wewe ni taa yangu, Ee BWANA.
BWANA hulifanya giza langu
kuwa mwanga.
30 Kwa msaada wako naweza kushinda
jeshi,
nikiwa pamoja na Mungu wangu
nitaweza kuruka ukuta.

31 [f]"Kuhusu Mungu, njia yake ni
kamilifu;
neno la BWANA halina dosari.
Yeye ni ngao kwa wote
wanaokimbilia kwake.
32 [g]Kwa maana ni nani aliye Mungu
zaidi ya BWANA?
Ni nani aliye Mwamba
isipokuwa Mungu wetu?
33 [h]Mungu ndiye anivikaye nguvu
na kufanya njia yangu kuwa
kamilifu.
34 [i]Huifanya miguu yangu kama miguu
ya kulungu,
huniwezesha kusimama mahali
palipo juu.
35 [j]Huifundisha mikono yangu
kupigana vita;
mikono yangu inaweza kupinda
upinde wa shaba.
36 [k]Hunipa ngao yako ya ushindi,
unajishusha chini ili kuniinua.
37 [l]Huyapanua mapito yangu,
ili miguu yangu isiteleze.

38 "Niliwafuatia adui zangu na
nikawaseta,
sikurudi nyuma mpaka
walipoangamizwa.
39 [m]Niliwaseta kabisa, nao hawakuweza
kuinuka tena;
walianguka chini ya miguu yangu.
40 [n]Ulinivika nguvu kwa ajili ya
kupigana vita;
uliwafanya adui zangu wasujudu
miguuni pangu.
41 [o]Uliwafanya adui zangu wageuke na
kukimbia,
nami nikawaangamiza adui zangu.
42 [p]Walipiga yowe, lakini hapakuwepo
na yeyote wa kuwaokoa;
walimlilia BWANA, lakini
hakuwajibu.
43 [q]Niliwaponda kama mavumbi ya
nchi;
niliwaponda na kuwakanyaga
kama tope barabarani.

44 [r]"Umeniokoa kutokana na
mashambulizi ya watu wangu;
umenihifadhi mimi kama kiongozi
wa mataifa.

---

[a]**22:26** Mt 5:7
[b]**22:27** Mt 5:8; Law 26:23-24
[c]**22:27** 1Nya 27:9-10
[d]**22:28** Kut 3:8; 1Sam 2:8-9; Za 72:12-13; Mit 30:13; Dan 4:31; Sef 3:11; Isa 2:12-17; 5:15; Za 12:5; Mt 5:3
[e]**22:29** Za 27:1; Isa 2:5; Mik 7:8; Ufu 21:23; 22:5
[f]**22:31** Kum 32:4; Mt 5:48; Za 12:6; 119:140; Mit 30:5-6; Mwa 15:1; Dan 4:37; Ufu 15:3
[g]**22:32** Kut 32:31; 1Sam 2:2; Isa 45:5-6
[h]**22:33** 1Sam 2:2; 2Sam 7:22; Za 27:1; Kum 18:13
[i]**22:34** Isa 35:6; Hab 3:19; Kum 32:13
[j]**22:35** Za 144:1; 7:12; 11:2; Zek 9:13
[k]**22:36** Efe 6:16
[l]**22:37** Mit 4:11
[m]**22:39** Za 44:5; 110:6; Mal 4:3
[n]**22:40** Yos 10:24; 1Fal 5:3; Za 44:5
[o]**22:41** Kut 23:27
[p]**22:42** Isa 1:15; Za 50:22; 1Sam 14:37; 28:6; Ay 27:6; Mit 1:28
[q]**22:43** 1Fal 20:10; 2Fal 13:7; Isa 41:2; Amo 1:3; Za 7:5; Isa 41:25; Mik 7:10; Zek 10:5; Isa 5:25; 10:6; 22:5
[r]**22:44** Kut 11:3; 2Sam 3:1; 8:1-14; Isa 55:3-5; Kum 28:13

Watu ambao sikuwajua
wananitumikia,
45 [a]nao wageni huja
wakininyenyekea,
mara wanisikiapo, hunitii.
46 [b]Wote wanalegea,
wanatoka katika ngome zao
wakitetemeka.

47 [c]"BWANA yu hai! Sifa ni kwa
Mwamba wangu!
Atukuzwe Mungu,
Mwamba, Mwokozi wangu!
48 [d]Yeye ndiye Mungu anilipiziaye
kisasi,
ayawekaye mataifa chini yangu,
49 [e]aniwekaye huru toka kwa adui
zangu.
Uliniinua juu ya adui zangu;
uliniokoa toka kwa watu wajeuri.
50 [f]Kwa hiyo nitakusifu, Ee BWANA,
katikati ya mataifa;
nitaliimbia sifa jina lako.
51 [g]Humpa mfalme wake ushindi mkuu;
huonyesha fadhili zake kwa
mpakwa mafuta wake,
kwa Daudi na wazao wake
milele."

*Maneno Ya Mwisho Ya Daudi*

23 [h]Haya ni maneno ya mwisho ya Daudi:

"Neno la Daudi mwana
wa Yese,
neno la mtu aliyeinuliwa na Aliye
Juu Sana,
mtu aliyepakwa mafuta na Mungu
wa Yakobo,
mwimbaji wa nyimbo wa Israeli:
2 [i]"Roho wa BWANA alinena kupitia
kwangu,
neno lake lilikuwa ulimini
mwangu.
3 [j]Mungu wa Israeli alinena,
mwamba wa Israeli akaniambia:
'Mtu anatawala watu kwa haki,
wakati anapotawala
akiwa na hofu ya Mungu,
4 [k]yeye ni kama mwanga wa asubuhi
jua lichomozapo
asubuhi isiyo na mawingu,
kama mwanga baada ya mvua
uchipuzao majani kutoka ardhini.'

5 [l]"Je, si hivyo ilivyo nyumba yangu
mbele za Mungu?
Je, hajafanya Agano la milele nami,
lililopangwa na kuimarishwa
kila sehemu?
Je, hatanifanya niufurahie wokovu
wangu
na kunijalia matakwa yangu yote?
6 [m]Lakini watu waovu wote
watatupwa kando kama miiba,
ambayo haikusanywi kwa mkono.
7 Yeyote agusaye miiba
hutumia chombo cha chuma
au mpini wa mkuki,
nayo huchomwa pale ilipo."

*Mashujaa Wa Daudi*

**(1 Nyakati 11:10-41)**

8 [n]Haya ndiyo majina ya mashujaa wa
Daudi:

Yosheb-Bashebethi,[o] Mtahkemoni, alikuwa kiongozi wa wale Watatu; yeye aliinua mkuki wake dhidi ya watu 800, ambao aliwaua katika pambano moja.

---

[a]**22:45** Za 66:3; 81:15; Kum 33:29
[b]**22:46** Mik 7:17
[c]**22:47** Kut 15:2; Kum 32:15; Za 18:31; 89:26; 95:1
[d]**22:48** Hes 31:3; Za 144:2; 1Sam 25:39; Za 94:1
[e]**22:49** Za 140:1; 27:6
[f]**22:50** Za 9:11; 47:6; 68:4; Rum 15:9
[g]**22:51** Za 21:1; 144:9-10; 1Sam 16; 13; Za 89:20; Mdo 13:23; 2Sam 7:13; Za 89:24, 29
[h]**23:1** Kut 11:3; Za 78:70-71; 89:27; 1Sam 2:10, 35; Za 18:50; 20:6; 84:9; Isa 45:1; Hab 3:13; 1Sam 16:12-13
[i]**23:2** Mt 22:43; Mk 12:36; 2Pet 1:21
[j]**23:3** Kum 32:4; 1Sam 2:2; Za 18:31; 72:3; Mwa 42:18; Isa 11:1-5; 2Nya 19:7-9; Kut 18:21
[k]**23:4** Yon 1:5; Za 119:147; 130:6; Mit 4:18; Amu 5:31; Mt 13:43; Kum 32:2
[l]**23:5** Mwa 9:16; Za 89:29; Isa 55:3
[m]**23:6** Isa 5:6; 9:18; 10:17; 27:4; 33:12; Mik 7:4; Nah 1:10; Mt 13:40-41
[n]**23:8** 2Sam 17:10; 1Nya 27:2
[o]8 Yosheb-Bashebethi au Yashobeamu (1Nya 11:11).

9 [a]Wa pili wake alikuwa Eleazari mwana
wa Dodai,[b] Mwahohi. Akiwa mmojawapo
wa wale mashujaa watatu, alikuwa pamoja
na Daudi wakati waliwadhihaki Wafilisti
waliokuwa wamekusanyika huko Pas-
Damimu kwa ajili ya vita. Kisha watu wa
Israeli wakarudi nyuma, 10 lakini yeye
alisimama imara akawaua Wafilisti hadi
mkono wake ukachoka na ukagandamana
na upanga. Bwana akawapa ushindi
mkubwa siku ile. Vikosi vikarudi kwa
Eleazari, kuteka tu nyara za waliokufa.

11 Aliyefuata alikuwa Shama mwana wa
Agee, Mharari. Wafilisti walipokusanyika
pamoja mahali palipokuwa shamba lililojaa
dengu, vikosi vya Israeli viliwakimbia.
12 Lakini Shama akasimama imara katikati
ya lile shamba. Akalitetea na kuwaua
Wafilisti, naye Bwana akawapa ushindi
mkubwa.

13 [c]Wakati wa mavuno, viongozi watatu
kati ya viongozi thelathini walishuka,
wakamwendea Daudi katika pango la
Adulamu, wakati kikundi cha Wafilisti
kilikuwa kimepiga kambi katika Bonde
la Warefai. 14 [d]Wakati huo Daudi alikuwa
katika ngome, na kambi ya Wafilisti ilikuwa
huko Bethlehemu. 15 Daudi akatamani maji,
akasema, “Laiti mtu angenipatia maji ya
kunywa kutoka kisima kilicho karibu na
lango la Bethlehemu!” 16 [e]Basi mashujaa
hao watatu wakapenya katikati ya Wafilisti,
wakaenda kuchota maji kutoka kwa kisima
kilicho karibu na lango la Bethlehemu,
wakamletea Daudi. Lakini Daudi akakataa
kuyanywa. Badala yake, aliyamimina mbele
za Bwana. 17 [fg]Akasema, “Iwe mbali nami,
Ee Bwana, kufanya kitu hiki. Je, hii si
damu ya watu ambao walikwenda kwa
kuhatarisha maisha yao?” Naye Daudi
hakuyanywa.

Haya yalifanywa na hao mashujaa
watatu.

18 [h]Abishai ndugu yake Yoabu mwana
wa Seruya ndiye alikuwa kiongozi wa
hao Watatu. Aliinua mkuki wake dhidi ya
watu 300 ambao aliwaua, kwa hiyo naye
akawa na sifa kama hao Watatu. 19 Je,
hakupata heshima kubwa zaidi kuliko hao
Watatu? Alikuwa jemadari wao, ingawa
hakuhesabiwa miongoni mwao.

20 [i]Benaya mwana wa Yehoyada alikuwa
mpiganaji hodari kutoka Kabseeli ambaye
alifanya mambo makubwa ya ujasiri.
Aliwaua mashujaa wawili waliokuwa
hodari kuliko wote wa Moabu. Pia
alishuka shimoni kulipokuwa na theluji
na kumuua simba. 21 [j]Pia alimuua Mmisri
mrefu mkubwa. Ingawa Mmisri alikuwa
na mkuki mkononi mwake, Benaya
alimwendea akiwa na rungu. Alipokonya
mkuki kutoka mkononi mwa Mmisri na
kumuua kwa mkuki wake mwenyewe.
22 Haya yalikuwa mambo ya ushujaa ya
Benaya mwana wa Yehoyada; naye pia
alikuwa maarufu kama wale mashujaa
watatu. 23 [k]Yeye aliheshimiwa zaidi ya wale
Thelathini, lakini hakujumuishwa miongoni
mwa wale Watatu. Daudi akamweka kuwa
kiongozi wa walinzi wake.

24 [l]Miongoni mwa wale Thelathini
walikuwepo:
Asaheli ndugu wa Yoabu;
Elhanani mwana wa Dodo kutoka
Bethlehemu;
25 [m]Shama, Mharodi;
Elika, Mharodi;
26 [n]Helesi, Mpalti;
Ira mwana wa Ikeshi kutoka
Tekoa;
27 Abiezeri kutoka Anathothi;

[a]**23:9** 1Nya 27:4; 8:4; 11:12
[b]9 Dodai tafsiri nyingine zinamwita Dodo.
[c]**23:13** Mwa 38:1; Yos 12:15; 17:18; 1Sam 22:1; 2Sam 5:18; 1Nya 11:15; 14:9; Kum 33:29; 1Nya 29:11; 2Nya 11:14; 25:8; Za 3:8; 46:1; Rum 8:31; Isa 17:5
[d]**23:14** 1Sam 22:4-5; 2Sam 5:17; Rut 1:19; 1Nya 12:16
[e]**23:16** Mwa 35:14
[f]**23:17** Law 17:10-12
[g]**23:17** Law 17:10
[h]**23:18** 1Sam 26:6; 1Nya 11:20; 2Sam 2:18
[i]**23:20** 2Sam 8:18; 1Nya 27:5; Yos 15:21; Kut 15:15
[j]**23:21** 1Nya 11:23
[k]**23:23** 2Sam 8:18
[l]**23:24** 2Sam 2:18
[m]**23:25** Amu 7:1; 1Nya 11:27
[n]**23:26** 1Nya 27:9-10

Mebunai, Mhushathi;
28 [a]Salmoni, Mwahohi;
Maharai, Mnetofathi;
29 [b]Heledi mwana wa Baana, Mnetofathi;
Itai mwana wa Ribai kutoka Gibea ya Benyamini;
30 [c]Benaya Mpirathoni;
Hidai kutoka mabonde ya Gaashi;
31 [d]Abi-Alboni, Mwaribathi;
Azmawethi, Mbarhumi;
32 Eliaba, Mshaalboni;
wana wa Yasheni;
Yonathani 33 mwana wa Shama, Mharari;
Ahiamu mwana wa Sharari, Mharari;
34 [e]Elifeleti mwana wa Ahasbai, Mmaakathi;
Eliamu mwana wa Ahithofeli, Mgiloni;
35 [f]Hezro, Mkarmeli;
Paarai, Mwarbi;
36 [g]Igali mwana wa Nathani kutoka Soba;
Bani, Mgadi;
37 [h]Seleki, Mwamoni;
Naharai, Mbeerothi, aliyekuwa mbeba silaha za Yoabu mwana wa Seruya;
38 [i]Ira, Mwithiri;
Garebu, Mwithiri;
39 [j]na Uria, Mhiti.
Jumla yao wote walikuwa watu thelathini na saba.

*Daudi Ahesabu Wapiganaji*

**(1 Nyakati 21:1-27)**

24 [k]Hasira ya BWANA ikawaka tena dhidi
ya Israeli, naye akamchochea Daudi
dhidi yao, akisema, "Nenda ukawahesabu
Israeli na Yuda."
2 [l]Kwa hiyo mfalme akamwambia Yoabu,
pamoja na majemadari wa jeshi aliokuwa
nao, "Nendeni kwa makabila yote ya
Israeli kuanzia Dani hadi Beer-Sheba na
mwandikishe watu wapiganaji, ili niweze
kujua idadi yao."
3 [m]Lakini Yoabu akamjibu mfalme,
"BWANA Mungu wako na azidishe jeshi
mara mia, nayo macho ya bwana wangu
mfalme na yaone hili. Lakini kwa nini
bwana wangu mfalme anataka kufanya
kitu cha namna hii?"
4 [n]Hata hivyo, neno la mfalme likawa na
nguvu juu ya Yoabu pamoja na majemadari
wa jeshi, kwa hiyo wakaondoka mbele ya
mfalme kuandikisha wapiganaji wa Israeli.
5 [o]Baada ya kuvuka Yordani, walipiga
kambi karibu na Aroeri, kusini ya mji ulioko
kwenye bonde jembamba, ndipo wakipitia
Gadi, wakaenda hadi Yazeri.
6 [p]Walikwenda
hadi Gileadi na pia eneo la Tahtimu-
Hodshi, wakaendelea hadi Dani-Yaani
na kuzunguka kuelekea Sidoni.
7 [q]Kisha
wakaenda kuelekea ngome ya Tiro pamoja
na miji yote ya Wahivi na ya Wakanaani.
Mwishoni, walikwenda mpaka Beer-Sheba
katika Negebu ya Yuda.
8 Baada ya kupita katika nchi nzima,
walirudi Yerusalemu baada ya miezi tisa
na siku ishirini.
9 [r]Yoabu akatoa hesabu ya wapiganaji

[a]**23:28** 1Nya 27:13; 2Fal 25:23; Ezr 2:22; Neh 7:26; Yer 40:8
[b]**23:29** 1Nya 27:15; Yos 15:57
[c]**23:30** Amu 12:13; Yos 24:30; Amu 2:9
[d]**23:31** 2Sam 3:16
[e]**23:34** Kum 3:14; 2Sam 11:3; 15:12
[f]**23:35** Yos 12:22
[g]**23:36** 1Sam 14:47
[h]**23:37** Yos 9:17
[i]**23:38** 1Nya 2:53; 2Sam 20:26; Yos 15:48
[j]**23:39** 2Sam 11:3
[k]**24:1** Yos 9:15; Ay 1:6; Zek 3:1; Kut 30:12; 1Nya 27:23; 2Sam 16:10; 21:11; 1Fal 22:22; 1Nya 21:1; Yak 1:13
[l]**24:2** 2Sam 20:23; 3:10; 2Nya 2:17; 17:14; 25:5; Amu 20:1; Mwa 26:4; Kum 8:13-14; 2Nya 32:25-26; Mit 18:12; 29:23; Yer 17:5
[m]**24:3** 2Sam 2:18; Kum 1:11
[n]**24:4** 1Nya 21:4; Mhu 8:4; Mdo 5:29
[o]**24:5** Yos 13:9; Hes 21:32; Kum 2:36
[p]**24:6** Mwa 10:19; Amu 1:31; Yos 19:28; Amu 18:28-29
[q]**24:7** Yos 19:29; Kut 3:8; Kum 1:31; Yos 11:3; Mwa 21:21-33
[r]**24:9** Hes 1:44-46; 1Nya 21:5

kwa mfalme: Katika Israeli kulikuwako
watu 800,000 wenye uwezo wa kupigana,
na katika Yuda watu 500,000.
10 [a]Dhamiri ya Daudi ilishtuka baada ya
kuwahesabu wapiganaji, naye akamwambia
BWANA, "Nimefanya dhambi kubwa kwa
kufanya jambo hili. Ee BWANA, sasa
ninakusihi, ondoa hatia ya mtumishi wako.
Nimefanya jambo la kipumbavu sana."
11 [b]Kabla Daudi hajaamka kesho yake
asubuhi, neno la BWANA lilikuwa limemjia
Gadi nabii, aliyekuwa mwonaji wa Daudi,
kusema: 12 "Nenda ukamwambie Daudi,
'Hivi ndivyo asemavyo BWANA: Ninakupa
wewe uchaguzi wa mambo matatu.
Nichagulie mojawapo nitakalotenda dhidi
yako.' "
13 [c]Basi Gadi akaenda kwa Daudi na
kumwambia, "Je, ije njaa ya miaka
mitatu katika nchi yako? Au miezi mitatu
ya kukimbia adui zako wakikufuatia?
Au siku tatu za tauni katika nchi yako?
Basi sasa, fikiri juu ya hilo na uamue jinsi
nitakavyomjibu huyo aliyenituma."
14 [d]Daudi akamjibu Gadi, "Nitataabika
sana. Afadhali tuangukie mikononi mwa
BWANA, kwa maana rehema zake ni kuu,
lakini usiniache nianguke mikononi mwa
wanadamu."
15 [e]Basi BWANA akatuma tauni katika
Israeli kuanzia asubuhi mpaka mwisho
wa muda ulioamriwa, wakafa watu 70,000
kuanzia Dani hadi Beer-Sheba. 16 [f]Malaika
aliponyoosha mkono wake ili kuangamiza
Yerusalemu, BWANA akahuzunika kwa
sababu ya maafa, akamwambia yule
malaika aliyekuwa anawadhuru watu,
"Yatosha! Rudisha mkono wako." Wakati
huo malaika wa BWANA alikuwa kwenye
sakafu ya kupuria ya Arauna,[g] Myebusi.
17 [h]Ikawa Daudi alipomwona huyo malaika
aliyekuwa akiwaua watu, akamwambia
BWANA, "Mimi ndiye niliyetenda dhambi
na kukosa. Hawa ni kondoo tu. Wamefanya
nini? Mkono wako uwe juu yangu na
nyumba yangu."

*Daudi Ajenga Madhabahu*

18 [i]Siku hiyo Gadi akamwendea Daudi na
kumwambia, "Panda ukamjengee BWANA
madhabahu kwenye sakafu ya kupuria
ya Arauna Myebusi." 19 Kwa hiyo Daudi
akakwea kama vile BWANA alivyokuwa
ameamuru kwa kinywa cha Gadi. 20 Arauna
alipotazama na kumwona mfalme na watu
wake wakija kumwelekea, alitoka nje na
kusujudu mbele ya mfalme kifudifudi,
akiuinamisha uso wake ardhini.
21 [j]Arauna akasema, "Mbona bwana
wangu mfalme amekuja kwa mtumishi
wake?"
Daudi akajibu, "Kununua sakafu yako
ya kupuria, ili niweze kumjengea BWANA
madhabahu, ili tauni iliyo katika watu
iondolewe."
22 [k]Arauna akamwambia Daudi, "Bwana
wangu mfalme na achukue chochote
kinachompendeza na akitoe sadaka.
Hapa kuna maksai kwa ajili ya sadaka ya
kuteketezwa, pia kuna miti ya kupuria na
nira za ng'ombe kwa ajili ya kuni. 23 [l]Ee
mfalme, Arauna anatoa vyote hivi kwa
mfalme." Pia Arauna akamwambia mfalme,
"BWANA Mungu wako na akukubali."
24 [m]Lakini mfalme akamjibu Arauna, "La
hasha, nasisitiza kuvilipia. Sitatoa sadaka
ya kuteketezwa kwa BWANA Mungu wangu
isiyonigharimu chochote."

---

[a]**24:10** 1Sam 24:5; Hes 22:34; 12:11; 2Sam 12:13; 1Sam 13:13; Mit 18:4; 1Yn 3:20; 1Nya 21:8; Ay 33:27-28; Za 25:11
[b]**24:11** 1Sam 22:5; 9:9; 1Nya 29:29
[c]**24:13** Kum 28:28-48; 32:24; Eze 14:21; Kut 5:3; 30:12; Law 26:25; Kum 28:21-28, 35; 1Nya 21:12
[d]**24:14** Neh 9:28; Za 4:1; 51:1; 103:8-13; Isa 54:7; 55:7; Yer 33:8; 42:12; Dan 9:9; Isa 47:6; Zek 1:15
[e]**24:15** 1Nya 24:24; 21:14; 27:24
[f]**24:16** Mwa 6:6; 16:7; 19:13; Kut 12:23; Mdo 12:23; 1Nya 21:15; Za 104:4; 1Sam 15:11; Za 78:38; Yer 18:5-10; Yoe 2:13; Yon 3:10
[g]16 Pia anaitwa Ornani kwa Kiebrania.
[h]**24:17** Za 74:1; 100:3; Yer 49:20; Mwa 18:23; Yon 1:12; 1Nya 21:17
[i]**24:18** Mwa 22:2; 2Nya 3:1
[j]**24:21** Hes 16:44-50; Mwa 23:8
[k]**24:22** 1Sam 6:14; 1Fal 19:21
[l]**24:23** Mwa 23:11; Eze 20:40-41; Za 20:3; 119:108; 1Pet 2:5
[m]**24:24** Mal 1:13-14; Mwa 23:16

Kwa hiyo Daudi akanunua ile sakafu ya kupuria nafaka na maksai, akazilipia shekeli hamsini za fedha.[a] 25 [b]Kisha Daudi akamjengea BWANA madhabahu mahali hapo, na kutoa sadaka za kuteketezwa na sadaka za amani. Kisha BWANA akajibu kwa ajili ya nchi, nayo tauni ikakoma katika Israeli.

---

[a]24 Shekeli 50 za fedha ni sawa na gramu 600.

[b]**24:25** 1Sam 7:17; 2Sam 21:14; 1Nya 21:28; 22:1; 2Sam 21:14; 2Nya 33:13

# 1 WAFALME

*Adoniya Ajitangaza Mfalme*

1 [a]Mfalme Daudi alipokuwa mzee umri
ukiwa umesogea, hakuweza kupata
joto hata walipomfunika kwa nguo. 2 [b]Kwa
hiyo watumishi wake wakamwambia,
“Turuhusu tumtafute kijana mwanamwali
bikira amhudumie mfalme na kumtunza.
Anaweza kulala pembeni mwake ili bwana
wetu mfalme apate joto.”
3 [c]Kisha wakatafuta katika Israeli yote
ili kumpata msichana mzuri wa sura
na wakampata Abishagi, Mshunami,
wakamleta kwa mfalme. 4 [d]Msichana huyo
alikuwa mzuri sana wa sura, akamtunza
mfalme na kumhudumia, lakini mfalme
hakufanya naye tendo la ndoa.
5 [e]Basi Adoniya, ambaye mama yake
alikuwa Hagithi, akajigamba na kusema,
“Mimi nitakuwa mfalme.” Hivyo akajiwekea
tayari magari na wapanda farasi, pamoja na
watu hamsini wa kumtangulia wakikimbia.
6 (Baba yake hakuwa ameingilia na
kumuuliza, “Kwa nini unafanya hivyo?”
Alikuwa pia kijana mzuri sana wa sura, na
alizaliwa baada ya Absalomu.)
7 [f]Adoniya akashauriana pamoja na Yoabu
mwana wa Seruya na kuhani Abiathari,
nao wakamsaidia. 8 [g]Lakini kuhani Sadoki,
Benaya mwana wa Yehoyada, Nathani
nabii, Shimei, Rei na walinzi maalum wa
Daudi hawakujiunga na Adoniya.
9 Ndipo Adoniya akatoa dhabihu ya
kondoo, ng’ombe na ndama walionona
kwenye Jiwe la Zohelethi karibu na
En-Rogeli. Akawaalika ndugu zake wote,
wana wa mfalme na wanaume wote wa
Yuda waliokuwa maafisa wa mfalme,
10 lakini hakumwalika nabii Nathani,
Benaya, walinzi maalum wa mfalme, wala
ndugu yake Solomoni.
11 Ndipo Nathani akamuuliza Bathsheba,
mama yake Solomoni, “Je, hujasikia
kwamba Adoniya, mwana wa Hagithi,
amekuwa mfalme pasipo bwana wetu
Daudi kujua jambo hili? 12 Sasa basi, acha
nikushauri jinsi utakavyookoa uhai wako
mwenyewe na uhai wa mwanao Solomoni.
13 Ingia kwa Mfalme Daudi na umwambie,
‘Bwana wangu mfalme, je hukuniapia
mimi mtumishi wako: “Hakika mwanao
Solomoni atakuwa mfalme baada yangu
na ndiye atakayeketi juu ya kiti changu cha
ufalme”? Kwa nini basi Adoniya amekuwa
mfalme?’ 14 Utakapokuwa ukizungumza
na mfalme, nitaingia na kuthibitisha hayo
uliyoyasema.”
15 Hivyo Bathsheba akaenda kumwona
mfalme chumbani mwake mahali
ambapo Abishagi, Mshunami, alikuwa
akimhudumia, naye mfalme alikuwa mzee
sana. 16 Bathsheba akasujudu na kupiga
magoti mbele ya mfalme.
Mfalme akauliza, “Ni nini hiki
unachotaka?”
17 Akamwambia, “Bwana wangu, wewe
mwenyewe uliniapia mimi mtumishi
wako kwa BWANA Mungu wako kwamba:
‘Solomoni Mwanao atakuwa mfalme baada
yangu na ndiye atakayeketi kwenye kiti
changu cha ufalme.’ 18 Lakini sasa Adoniya
amekuwa mfalme, nawe, bwana wangu
mfalme huna habari kuhusu jambo hilo.
19 Ametoa dhabihu idadi kubwa ya ng’ombe,
ndama walionona na kondoo, naye
amewaalika wana wa mfalme wote, kuhani
Abiathari, na Yoabu jemadari wa jeshi,
lakini hakumwalika Solomoni mtumishi
wako. 20 Bwana wangu mfalme, macho ya
Israeli yote yanakutazama wewe wajue
kutoka kwako kuwa ni nani atakayeketi
katika kiti cha ufalme cha bwana wangu
mfalme baada yake. 21 Kama sivyo, mara tu

[a]**1:1** Yer 29:10-14; Zek 1:12-16; 2Nya 36:22-23; Ezr 5:13; 7:27; Yer 25:12; Law 26:42
[b]**1:2** Amu 4:10; Isa 44:28; Ezr 5:13; Za 72:11
[c]**1:3** Kum 3:24; 2Sam 22:32; Za 86:10; Dan 6:26; 1Kor 8:6; Isa 37:16; Mk 12:32
[d]**1:4** Isa 10:20-22; Hes 15:3; Za 116:17; Ezr 3:7; 4:3
[e]**1:5** 2Nya 34:9; Neh 12:34; Hag 1:4; Mit 16:1
[f]**1:7** 2Fal 24:13; Ezr 5:14; 6:5; 2Nya 36:7; Yer 52:17-19
[g]**1:8** Ezr 5:14; Hag 1:1; 1Nya 3:18

bwana wangu mfalme atakapopumzishwa
pamoja na baba zake, mimi na mwanangu
Solomoni tutatendewa kama wahalifu.”
22 Alipokuwa angali anazungumza
na mfalme, nabii Nathani akafika.
23 Wakamwambia mfalme, “Nabii Nathani
yuko hapa.” Kisha akaenda mbele ya
mfalme na kumsujudia hadi uso wake
ukagusa ardhi.
24 Nathani akasema, “Je, bwana wangu
mfalme, umetangaza kuwa Adoniya
atakuwa mfalme baada yako na kwamba
ataketi kwenye kiti chako cha ufalme?
25 Leo ameshuka na kutoa dhabihu idadi
kubwa ya ng’ombe, ndama walionona
na kondoo. Amewaalika wana wote wa
mfalme, jemadari wa jeshi na kuhani
Abiathari. Sasa hivi, wanakula na kunywa
pamoja naye wakisema, ‘Aishi maisha
marefu, Mfalme Adoniya!’ 26 Lakini mimi
mtumishi wako, kuhani Sadoki, Benaya
mwana wa Yehoyada na mtumishi wako
Solomoni hakutualika. 27 Je, hili ni jambo
ambalo bwana wangu mfalme amelifanya
pasipo kuwajulisha watumishi wake ili
wapate kujua ni nani atakayeketi kwenye
kiti cha ufalme cha bwana wangu mfalme
baada yake?”

*Daudi Amfanya Solomoni Kuwa Mfalme*

28 Ndipo Mfalme Daudi akasema, “Mwite
Bathsheba, aingie ndani.” Hivyo akaingia
mbele ya mfalme na kusimama mbele yake.
29 Ndipo mfalme akaapa: “Hakika kama
BWANA aishivyo, ambaye ameniokoa
kutoka kila taabu, 30 hakika nitatekeleza leo
kile nilichokuapia kwa BWANA, Mungu wa
Israeli: Mwanao Solomoni atakuwa mfalme
baada yangu, naye ataketi kwenye kiti
changu cha ufalme baada yangu.”
31 Kisha Bathsheba akasujudu akipiga
magoti mbele ya mfalme uso wake ukigusa
ardhi akasema, “Bwana wangu Mfalme
Daudi na aishi milele!”
32 Mfalme Daudi akasema, “Mwite kuhani
Sadoki ndani, nabii Nathani na Benaya
mwana wa Yehoyada.” Walipofika mbele
ya mfalme, 33 akawaambia: “Wachukueni
watumishi wa bwana wenu pamoja nanyi na
mkamkalishe mwanangu Solomoni juu ya
nyumbu wangu mwenyewe mkamteremshe
hadi Gihoni. 34 Huko kuhani Sadoki na nabii
Nathani wamtie mafuta awe mfalme juu ya
Israeli. Pigeni tarumbeta na mpaze sauti,
‘Mfalme Solomoni aishi maisha marefu!’
35 Kisha mtapanda pamoja naye, atakuja na
kuketi kwenye kiti changu cha ufalme na
kutawala badala yangu. Nimemweka awe
mtawala juu ya Israeli na Yuda.”
36 Benaya mwana wa Yehoyada akamjibu
mfalme, “Amen! BWANA, Mungu wa bwana
wangu mfalme, na aseme vivyo hivyo.
37 Kama vile BWANA alivyokuwa na bwana
wangu mfalme, vivyo hivyo na awe na
Solomoni kukifanya kiti chake cha utawala
kuwa kikuu kuliko kile cha bwana wangu
Mfalme Daudi!”
38 Hivyo kuhani Sadoki, nabii Nathani,
Benaya mwana wa Yehoyada, Wakerethi
na Wapelethi wakampandisha Solomoni
juu ya nyumbu wa Mfalme Daudi, nao
wakamsindikiza hadi Gihoni. 39 Kuhani
Sadoki akachukua pembe ya mafuta kutoka
kwenye hema takatifu na kumtia Solomoni
mafuta. Kisha wakapiga tarumbeta na watu
wote wakapaza sauti wakisema, “Mfalme
Solomoni aishi maisha marefu!” 40 Na watu
wote wakakwea wakimfuata, wakipiga
filimbi na kushangilia sana, hata ardhi
ikatikisika kwa ile sauti.
41 Adoniya pamoja na wageni wote
waliokuwa pamoja naye wakasikia sauti
hiyo walipokuwa wakimalizia karamu yao.
Waliposikia sauti ya tarumbeta, Yoabu
akauliza, “Nini maana ya makelele yote
haya katika mji?”
42 Hata alipokuwa anasema, Yonathani
mwana wa kuhani Abiathari akafika.
Adoniya akasema, “Ingia ndani. Mtu
mstahiki kama wewe ni lazima alete habari
njema.”
43 Yonathani akajibu, “La hasha! Mfalme
Daudi bwana wetu amemfanya Solomoni
kuwa mfalme. 44 Mfalme amemtuma
pamoja naye kuhani Sadoki, nabii Nathani,
Benaya mwana wa Yehoyada, Wakerethi
na Wapelethi, nao wamempandisha juu
ya nyumbu wa mfalme, 45 nao kuhani
Sadoki na nabii Nathani wamemtia mafuta
kuwa mfalme huko Gihoni. Kuanzia hapo

wameendelea kushangilia na sauti zimeenea
pote mjini. Hizo ndizo kelele unazosikia.
46 Zaidi ya hayo, Solomoni ameketi juu ya
kiti chake cha ufalme. 47 Pia, maafisa wa
mfalme wamekuja ili kumtakia heri bwana
wetu Mfalme Daudi wakisema, 'Mungu
wako na alifanye jina la Solomoni kuwa
mashuhuri kuliko lako na kiti chake cha
ufalme kiwe na ukuu kuliko chako!' Naye
mfalme akasujudu akiabudu kitandani
mwake 48 na kusema, 'Ahimidiwe BWANA,
Mungu wa Israeli, ambaye ameruhusu
macho yangu kuona mrithi juu ya kiti
changu cha ufalme leo hii.' "

49 Katika hili, wageni wote wa Adoniya
wakainuka kwa mshtuko wa hofu na
kutawanyika. 50 Lakini Adoniya kwa
kumwogopa Solomoni, akaenda na kushika
pembe za madhabahu. 51 Kisha Solomoni
akaambiwa, "Adoniya anamwogopa
Mfalme Solomoni na ameshikilia pembe za
madhabahu. Anasema, 'Mfalme Solomoni
na aniapie leo kwamba hatamuua mtumishi
wake kwa upanga.' "

52 Solomoni akajibu, "Kama akijionyesha
kuwa mtu mstahiki, hakuna unywele wake
utakaoanguka juu ya ardhi, lakini kama
uovu ukionekana ndani yake, atakufa."
53 Ndipo Mfalme Solomoni akawatuma watu,
nao wakamshusha kutoka madhabahuni.
Naye Adoniya akaja akamwinamia Mfalme
Solomoni, naye Solomoni akamwambia,
"Nenda nyumbani kwako."

### *Maagizo Ya Daudi Kwa Solomoni*

2 [a]Siku zilipokaribia za Daudi kufa, akampa
mwanawe Solomoni agizo.

2 [b]Akasema, "Mimi ninakaribia kwenda
njia ya dunia yote. Hivyo uwe hodari,
jionyeshe kuwa mwanaume, 3 [c]shika lile
BWANA Mungu wako analokuagiza: Enenda
katika njia zake, ushike maagizo na amri
zake, sheria zake na kanuni zake, kama
ilivyoandikwa katika Sheria ya Mose, ili
upate kustawi katika yote ufanyayo na
popote uendako, 4 ili kwamba BWANA
aweze kunitimizia ahadi yake: 'Kama wazao
wako wakiangalia sana wanavyoishi, na
kama wakienenda kwa uaminifu mbele
zangu kwa mioyo yao yote na kwa roho
zao zote, kamwe hutakosa kuwa na mtu
kwenye kiti cha ufalme cha Israeli.'

5 [d]"Sasa wewe mwenyewe unafahamu
lile Yoabu mwana wa Seruya alilonitendea,
lile alilofanya kwa majemadari wawili wa
majeshi ya Israeli, Abneri mwana wa Neri,
na Amasa mwana wa Yetheri. Aliwaua,
akimwaga damu yao wakati wa amani
kama vile ni kwenye vita, tena akaipaka
damu ile kwenye mkanda uliokuwa kiunoni
mwake na viatu alivyovaa miguuni mwake.
6 Shughulika naye kwa kadiri ya hekima
yako, lakini usiache kichwa chake chenye
mvi kishukie kaburi kwa amani.

7 "Lakini uwaonyeshe wema wana wa
Barzilai wa Gileadi na uwaruhusu wawe
miongoni mwa wale walao mezani pako.
Walisimama nami nilipomkimbia ndugu
yako Absalomu.

8 "Ukumbuke, unaye Shimei mwana
wa Gera, Mbenyamini kutoka Bahurimu,
ambaye alinilaani kwa laana kali siku
niliyokwenda Mahanaimu. Aliposhuka
kunilaki huko Yordani, nilimwapia kwa
BWANA: 'Sitakuua kwa upanga!' 9 Lakini
sasa, usidhani kwamba hana hatia. Wewe
ni mtu wa hekima, utajua la kumtendea.
Zishushe mvi zake kaburini kwa damu."

10 Kisha Daudi akapumzika pamoja na
baba zake naye akazikwa katika Mji wa
Daudi. 11 Daudi alikuwa ametawala juu
ya Israeli miaka arobaini: huko Hebroni
alitawala miaka saba, na katika Yerusalemu
akatawala miaka thelathini na mitatu.
12 Kwa hiyo Solomoni akaketi katika kiti cha
ufalme cha baba yake Daudi, nao utawala
wake ukaimarika sana.

### *Kiti Cha Ufalme Cha Solomoni Chaimarishwa*

13 [e]Basi Adoniya, mwana wa Hagithi,
akaenda kwa Bathsheba, mama yake
Solomoni. Bathsheba akamuuliza, "Je,
umekuja kwa amani?"

---

[a]**2:1** 2Nya 36:20; Neh 7:6; 11:3; 2Fal 24:16;
25:12; Ezr 5:8; 6:2; Es 1:1; 8:9
[b]**2:2** 1Nya 3:19; 6:14; Hag 2:4; Zek 3:1-10
[c]**2:3** Ezr 10:25; Neh 3:25
[d]**2:5** Neh 6:18
[e]**2:13** Ezr 8:13; 7:18

Akajibu, “Ndiyo, kwa amani.” 14 Kisha
akaongeza, “Ninalo jambo la kukuambia.”
Akajibu, “Waweza kulisema.”
15 Akasema, “Kama unavyojua, ufalme
ulikuwa wangu. Israeli wote waliniangalia
mimi kama mfalme wao. Lakini mambo
yalibadilika, ufalme umekwenda kwa
ndugu yangu, kwa maana umemjia kutoka
kwa Bwana. 16 Sasa ninalo ombi moja
ninalokuomba. Usinikatalie.”
Bathsheba akasema, “Waweza kuliomba.”
17 Kwa hiyo akaendelea kusema,
“Tafadhali mwombe Mfalme Solomoni,
anipatie Abishagi, Mshunami, awe mke
wangu; hatakukatalia wewe.”
18 Bathsheba akamjibu, “Vema sana,
nitazungumza na mfalme kwa ajili yako.”
19 Bathsheba alipokwenda kwa Mfalme
Solomoni kuzungumza naye kwa ajili ya
Adoniya, mfalme alisimama kumlaki mama
yake, akamwinamia na kuketi kwenye kiti
chake cha ufalme. Akaamuru kiti cha ufalme
kuletwa kwa ajili ya mama yake mfalme,
naye akaketi mkono wake wa kuume.
20 [a]Bathsheba akamwambia mfalme,
“Ninalo ombi moja dogo la kukuomba;
usinikatalie.”
Mfalme akajibu, “Omba, mama yangu;
sitakukatalia.”
21 [b]Akasema, “Mruhusu Abishagi,
Mshunami, aolewe na ndugu yako Adoniya.”
22 Mfalme Solomoni akamjibu mama yake,
“Kwa nini uombe Abishagi, Mshunami, kwa
ajili ya Adoniya? Ungeweza pia kuomba
ufalme kwa ajili yake, kwani yeye ni ndugu
yangu mkubwa: naam, kwa ajili yake, na
kwa kuhani Abiathari na Yoabu mwana wa
Seruya!”
23 Mfalme Solomoni akaapa kwa Bwana,
akasema: “Mungu na aniulie mbali, tena
bila huruma, ikiwa Adoniya hatalipa kwa
uhai wake kwa ajili ya ombi hili! 24 Basi
sasa, hakika kama Bwana aishivyo, yeye
ambaye ameniimarisha salama kwenye
kiti cha ufalme cha Daudi baba yangu,
naye amenipa ufalme wa kudumu kama
alivyoahidi, Adoniya atauawa leo!” 25 Hivyo
Mfalme Solomoni akatoa amri kwa Benaya
mwana wa Yehoyada, naye akampiga
Adoniya akafa.
26 [c]Mfalme akamwambia kuhani
Abiathari, “Nenda huko Anathothi katika
mashamba yako. Wewe unastahili kufa,
lakini sitakuua sasa, kwa sababu ulilichukua
Sanduku la Bwana Mwenyezi mbele ya
Daudi baba yangu na ulishiriki taabu
zote za baba yangu.” 27 Hivyo Solomoni
akamwondoa Abiathari kwenye ukuhani
wa Bwana, akilitimiza neno la Bwana
alilokuwa amenena huko Shilo kuhusu
nyumba ya Eli.
28 [d]Habari zilipomfikia Yoabu, ambaye
alikuwa amefanya shauri baya na Adoniya,
lakini sio na Absalomu, alikimbilia kwenye
hema la Bwana na kushika pembe za
madhabahu. 29 Mfalme Solomoni akaambiwa
kuwa Yoabu amekimbilia kwenye hema la
Bwana naye alikuwa kando ya madhabahu.
Basi Solomoni akamwagiza Benaya mwana
wa Yehoyada: “Nenda ukamuue!”
30 Ndipo Benaya akaingia kwenye hema
la Bwana na kumwambia Yoabu, “Mfalme
anasema, ‘Toka nje!’ ”
Lakini akajibu, “La! Nitafia hapa hapa.”
Benaya akamwarifu mfalme, “Hivi
ndivyo Yoabu alivyonijibu.”
31 [e]Kisha mfalme akamwamuru Benaya,
“Fanya kama asemavyo. Muue na kumzika,
ili uniondolee mimi na nyumba ya baba
yangu dhambi ya damu isiyokuwa na
hatia ile Yoabu aliyoimwaga. 32 Bwana
atamlipiza kwa ajili ya damu aliyoimwaga,
kwa sababu pasipo Daudi baba yangu kujua,
aliwashambulia watu wawili na kuwaua
kwa upanga. Wote wawili, Abneri mwana
wa Neri, jemadari wa jeshi la Israeli, na
Amasa mwana wa Yetheri, jemadari wa
jeshi la Yuda, walikuwa watu wazuri na
wanyofu kuliko yeye. 33 Hatia ya damu
yao na iwe juu ya kichwa cha Yoabu na
wazao wake milele. Lakini kwa Daudi na
uzao wake, nyumba yake na kiti chake cha
ufalme, iwepo amani ya Bwana milele.”

[a]**2:20** Yos 9:17
[b]**2:21** Mik 5:2; 1Nya 2:51; Rut 1:19; Mt 2:6; 2Sam 21:2; Mwa 35:19
[c]**2:26** Yos 21:18; 1Sam 22:20; 2Sam 15:14
[d]**2:28** Mwa 12:8
[e]**2:31** Ezr 2:7

34 [a]Basi Benaya mwana wa Yehoyada
akakwea, akampiga na kumuua Yoabu,
naye akazikwa katika nchi yake mwenyewe
katika jangwa. 35 Mfalme akamweka Benaya
mwana wa Yehoyada juu ya jeshi kwenye
nafasi ya Yoabu na kumweka kuhani Sadoki
badala ya Abiathari.
36 [b]Kisha mfalme akatuma ujumbe kwa
Shimei na kumwambia, “Ujijengee nyumba
huko Yerusalemu uishi huko, lakini
usiende mahali pengine popote. 37 [c]Siku
utakayoondoka kuvuka Bonde la Kidroni,
uwe na hakika utakufa; damu yako itakuwa
juu ya kichwa chako mwenyewe.”
38 [d]Shimei akamjibu mfalme, “Ulilolisema
ni jema. Mtumishi wako atatenda kama
bwana wangu mfalme alivyosema.” Naye
Shimei akakaa Yerusalemu kwa muda
mrefu.
39 [e]Lakini baada ya miaka mitatu,
watumwa wawili wa Shimei wakatoroka
kwenda kwa Akishi mwana wa Maaka,
mfalme wa Gathi, naye Shimei akaambiwa,
“Watumwa wako wako Gathi.” 40 [f]Kwa ajili
ya hili, Shimei akatandika punda wake,
akaenda kwa Akishi huko Gathi kuwatafuta
watumwa wake. Basi Shimei akaondoka na
kuwarudisha watumwa wake kutoka Gathi.
41 [g]Solomoni alipoambiwa kuwa Shimei
ametoka Yerusalemu na kwenda Gathi na
amekwisha kurudi, 42 [h]mfalme akamwita
Shimei na kumwambia, “Je, sikukuapiza
kwa Bwana na kukuonya kuwa, ‘Siku
utakayoondoka kwenda mahali pengine
popote, uwe na hakika utakufa?’ Wakati ule
uliniambia, ‘Ulilolisema ni jema. Nitatii!’
43 [i]Kwa nini basi hukutunza kiapo chako
kwa Bwana na kutii amri niliyokupa?”
44 Pia mfalme akamwambia Shimei,
“Unajua katika moyo wako makosa
uliyomtendea baba yangu Daudi. Sasa
Bwana atakulipiza kwa ajili ya mabaya
yako uliyotenda. 45 Lakini Mfalme Solomoni
atabarikiwa, na kiti cha ufalme cha Daudi
kitakuwa imara mbele za Bwana milele.”
46 Kisha mfalme akatoa amri kwa Benaya
mwana wa Yehoyada, naye akatoka nje,
akampiga Shimei na kumuua.
Sasa ufalme ukawa umeimarika
kikamilifu mikononi mwa Solomoni.

*Solomoni Anaomba Hekima*

**(2 Nyakati 1:3-12)**

3 [j]Solomoni akafanya urafiki na Mfalme
Farao wa Misri na kumwoa binti yake.
Akamleta huyo binti katika Mji wa Daudi
mpaka alipomaliza kujenga jumba lake la
kifalme na Hekalu la Bwana, pamoja na
ukuta kuzunguka Yerusalemu. 2 Hata hivyo,
watu bado walikuwa wakitoa dhabihu
huko kwenye vilima, kwa sababu Hekalu
lilikuwa bado halijajengwa kwa ajili ya Jina
la Bwana. 3 [k]Solomoni akaonyesha upendo
wake kwa Bwana kwa kuenenda sawasawa
na amri za Daudi baba yake, ila yeye alitoa
dhabihu na kufukiza uvumba huko mahali
pa juu.
4 [l]Mfalme akaenda Gibeoni kutoa
dhabihu, kwa maana ndipo palipokuwa
mahali pa juu pa kuabudia, naye Solomoni
akatoa sadaka elfu moja za kuteketezwa juu
ya hayo madhabahu. 5 [m]Bwana akamtokea
Solomoni huko Gibeoni wakati wa usiku
katika ndoto, naye Mungu akasema, “Omba
lolote utakalo nikupe.”
6 Solomoni akajibu, “Umemfanyia
mtumishi wako, baba yangu Daudi, fadhili
nyingi, kwa kuwa alikuwa mwaminifu
kwako na mwenye haki, tena mnyofu wa
moyo. Nawe umemzidishia fadhili hii kuu
kwani umempa mwana wa kuketi kwenye
kiti chake cha ufalme, kama ilivyo leo.

[a]**2:34** Kum 34:3; 2Nya 28:15; 1Fal 16:34
[b]**2:36** 1Nya 9:10; 24:7
[c]**2:37** 1Nya 24:14; Ezr 10:20
[d]**2:38** 1Nya 9:12; Ezr 10:22
[e]**2:39** 1Nya 24:8
[f]**2:40** Hes 3:9; Ezr 3:9
[g]**2:41** 1Nya 15:16
[h]**2:42** 1Sam 3:15; 1Nya 9:17
[i]**2:43** 1Nya 9:2
[j]**3:1** Neh 7:73; Law 23:24
[k]**3:3** Kut 29:38-42; Hes 28:1-8; Dan 9:25; Ezr 4:4
[l]**3:4** Kut 23:16; Zek 14:16; Hes 29:12-38; Neh 8:14
[m]**3:5** Hes 28:3-11; Kol 2:16; Kut 29:38; Law 23:1-44; Hes 29:39

7 [a]“Sasa, Ee BWANA Mungu wangu,
umemfanya mtumishi wako mfalme badala
ya baba yangu Daudi. Lakini mimi ni mtoto
mdogo tu, wala sijui jinsi ya kutekeleza
wajibu wangu. 8 [b]Mtumishi wako yuko
hapa miongoni mwa watu uliowachagua:
taifa kubwa, watu wengi wasioweza
kuhesabika wala kutoa idadi yao. 9 [c]Hivyo
mpe mtumishi wako moyo wa ufahamu ili
kutawala watu wako na kupambanua kati
ya mema na mabaya. Kwa maana, ni nani
awezaye kutawala watu wako hawa walio
wengi hivi?”

10 [d]Bwana akapendezwa kwamba Solomoni
ameliomba jambo hili. 11 [e]Basi Mungu
akamwambia, “Kwa kuwa umeomba neno
hili na hukuomba maisha marefu au upate
utajiri kwa nafsi yako, wala adui zako wafe,
bali umeomba ufahamu katika kutoa haki,
12 [f]nitafanya lile uliloomba. Nitakupa moyo
wa hekima na wa ufahamu, kiasi kwamba
hajakuwepo mtu mwingine kama wewe,
wala kamwe hatakuwepo baada yako.
13 [g]Zaidi ya hayo, nitakupa yale ambayo
hukuomba, yaani utajiri na heshima, ili
kwamba maisha yako yote hapatakuwa na
mtu kama wewe miongoni mwa wafalme.
14 Nawe kama ukienenda katika njia zangu
na kutii sheria na amri zangu kama baba
yako Daudi alivyofanya, nitakupa maisha
marefu.” 15 Ndipo Solomoni akaamka,
akatambua kuwa ilikuwa ndoto.

Akarudi Yerusalemu, akasimama mbele ya Sanduku la Agano la BWANA, naye akatoa dhabihu za kuteketezwa na sadaka za amani. Kisha akawafanyia watumishi wake wote karamu.

*Utawala Wa Hekima*

16 Basi wanawake wawili makahaba
walikuja kwa mfalme na kusimama
mbele yake. 17 Mmojawapo akasema,
“Bwana wangu, mimi na mwanamke huyu
tunaishi kwenye nyumba moja. Nilikuwa
nimezaa alipokuwa pamoja nami. 18 Siku
ya tatu baada ya mtoto wangu kuzaliwa,
mwanamke huyu pia naye akazaa mtoto.
Tulikuwa peke yetu, hapakuwa na mtu
mwingine yeyote katika nyumba isipokuwa
sisi wawili.

19 “Wakati wa usiku mwana wa huyu
mwanamke akafa kwa sababu alimlalia.
20 Hivyo akaondoka katikati ya usiku na
kumchukua mwanangu kutoka ubavuni
pangu wakati mimi mtumishi wako
nilipokuwa nimelala. Akamweka kifuani
mwake na kumweka mwanawe aliyekufa
kifuani mwangu. 21 Asubuhi yake, nikaamka
ili kumnyonyesha mwanangu, naye
alikuwa amekufa! Lakini nilipomwangalia
sana katika nuru ya asubuhi, niliona
kuwa hakuwa yule mwana niliyekuwa
nimemzaa.”

22 Huyo mwanamke mwingine akasema,
“Hapana! Mwana aliye hai ndiye wangu,
aliyekufa ni wako.”

Lakini yule wa kwanza akasisitiza, “Hapana! Mwana aliyekufa ni wako, aliye hai ni wangu.” Hivi ndivyo walivyobishana mbele ya mfalme.

23 Mfalme akasema, “Huyu anasema,
‘Mwanangu ndiye aliye hai, na aliyekufa
ndiye mwanao,’ maadamu yule anasema,
‘Hapana! Aliyekufa ni wako, na aliye hai
ni wangu.’ ”

24 Kisha mfalme akasema, “Nileteeni
upanga.” Basi wakamletea mfalme upanga.
25 Ndipo mfalme akatoa amri: “Mkate mtoto
aliye hai vipande viwili; mpe huyu nusu na
mwingine nusu.”

26 Mwanamke ambaye mwanawe
alikuwa hai akajawa na huruma kwa ajili
ya mwanawe na kumwambia mfalme,
“Tafadhali, bwana wangu, mpe yeye mtoto
aliye hai! Usimuue!”

Lakini yule mwanamke mwingine akasema, “Mkate vipande viwili. Asiwe wangu au wake!”

[a]**3:7** 1Nya 14:1; Isa 35:2; Ezr 6:3; 2Nya 2:10; Mdo 9:36; 12:20; Isa 60:13
[b]**3:8** Zek 4:9; Hes 4:3; 1Nya 23:24-27
[c]**3:9** Ezr 2:40
[d]**3:10** Zek 6:12; Ezr 6:3; 1Nya 15:27-28; 6:31; Hag 2:15; 2Nya 5:13; 1Nya 6:31
[e]**3:11** 1Nya 16:34; Za 138:8; Yos 6:5-10; Neh 12:24; 2Nya 7:3; Yer 33:11; Lk 1:50; Za 136:1; Kut 15:21
[f]**3:12** Hag 2:3-9
[g]**3:13** Yer 48:33

27 Kisha mfalme akatoa uamuzi wake:
“Mpeni mama wa kwanza mtoto aliye hai.
Msimuue; ndiye mama yake.”
28 Wakati Israeli yote iliposikia hukumu
aliyotoa mfalme, wakamwogopa mfalme,
kwa sababu waliona kuwa alikuwa na
hekima kutoka kwa Mungu kwa kutoa haki.

*Maafisa Wa Solomoni Na Watawala*

4 Basi Mfalme Solomoni akatawala Israeli
yote. 2 [a]Hawa ndio waliokuwa maafisa
wake wakuu:

Kuhani: Azaria mwana wa Sadoki;
3 [b]Elihorefu na Ahiya, wana wa Shisha: waandishi;
Yehoshafati mwana wa Ahiludi: karani;
4 [c]Benaya mwana wa Yehoyada: jemadari mkuu wa jeshi;
Sadoki na Abiathari: makuhani;
5 Azaria mwana wa Nathani: kiongozi wa maafisa wa wilaya;
Zabudi mwana wa Nathani: kuhani na mshauri binafsi wa mfalme;
6 [d]Ahishari: msimamizi wa jumba la kifalme;
Adoniramu mwana wa Abda: msimamizi wa kazi za kulazimisha.

7 [e]Pia Solomoni alikuwa na watawala
kumi na wawili wa wilaya katika Israeli
yote, walioleta mahitaji kwa mfalme na
kwa watu wa nyumbani kwa mfalme. Kila
mmoja alitoa chakula kwa mwezi mmoja
katika mwaka. 8 [f]Majina yao ni haya:

Ben-Huri: katika nchi ya vilima ya Efraimu;
9 [g]Ben-Dekeri: katika Makasi, Shaalbimu, Beth-Shemeshi na Elon-Bethhanani;
10 [h]Ben-Hesedi: katika Arubothi (Soko na nchi yote ya Heferi zilikuwa zake);
11 Ben-Abinadabu: katika Nafoth-Dori (alimwoa Tafathi binti Solomoni);
12 [i]Baana mwana wa Ahiludi: katika Taanaki na Megido, na katika Beth-Shani yote karibu na Sarethani chini ya Yezreeli, kuanzia Beth-Shani hadi Abel-Mehola kupita hadi Yokmeamu;
13 [j]Ben-Geberi: katika Ramoth-Gileadi (makao ya Yairi mwana wa Manase katika Gileadi ilikuwa miji yake, pamoja na wilaya ya Argobu katika Bashani na miji yake mikubwa sitini yenye kuzungukwa na kuta zenye makomeo ya shaba);
14 Ahinadabu mwana wa Ido: katika Mahanaimu;
15 [k]Ahimaasi: katika Naftali (alikuwa amemwoa Basemathi binti Solomoni);
16 Baana mwana wa Hushai: katika Asheri na katika Bealothi;
17 Yehoshafati mwana wa Parua: katika Isakari;
18 Shimei mwana wa Ela: katika Benyamini;
19 [l]Geberi mwana wa Uri: katika Gileadi (nchi ya Sihoni mfalme wa Waamori na nchi ya Ogu mfalme wa Bashani). Naye alikuwa ndiye mtawala pekee katika eneo hilo.

*Mahitaji Ya Solomoni Ya Kila Siku*

20 [m]Watu wa Yuda na Israeli walikuwa
wengi kama mchanga wa pwani; walikula,
wakanywa na kufurahi. 21 Mfalme Solomoni
akatawala katika falme zote kuanzia Mto
Frati hadi nchi ya Wafilisti, hadi kwenye
mpaka wa Misri. Nchi hizi zilileta ushuru

[a]**4:2** Es 8:17; 2Fal 17:24, 41; 19:37
[b]**4:3** Yn 4:9; 2Nya 36:22-23; Ezr 1:1-4; 6:3; Isa 44:28; Neh 2:20; Mdo 8:21
[c]**4:4** Ezr 3:3; Yer 38:4; Isa 35:3-4
[d]**4:6** Es 3:13; 9:5; Dan 9:1
[e]**4:7** Ezr 7:1; Isa 36:11; Neh 2:1
[f]**4:8** Za 112:6; Zek 1:14; Rum 8:28
[g]**4:9** Ezr 5:6; 2Fal 17:30, 31
[h]**4:10** Neh 4:2; Ezr 7:12
[i]**4:12** Amo 7:10; Lk 23:2; Mdo 24:5
[j]**4:13** Ezr 7:24; Neh 5:4; Mt 9:9
[k]**4:15** Ezr 5:17; Es 3:8; Mdo 17:6-7
[l]**4:19** 2Fal 18:7
[m]**4:20** Mwa 15:18-21; Kut 23:31; Za 72:8; 1Nya 18:3

na zilikuwa chini ya Solomoni, siku zote
za maisha yake.
22 [a]Mahitaji ya Solomoni ya kila siku
yalikuwa kori thelathini[b] za unga laini, kori
sitini[c] za unga wa kawaida. 23 [d]Ng'ombe kumi
wa zizini, ng'ombe ishirini wa malisho,
kondoo na mbuzi mia moja, pamoja na
ayala, paa, kulungu na kuku wazuri sana.
24 [e]Kwa kuwa Solomoni alitawala falme zote
magharibi ya mto, kuanzia Tifsa hadi Gaza,
naye akawa na amani pande zote. 25 Wakati
wa maisha ya Solomoni Yuda na Israeli,
kuanzia Dani mpaka Beer-Sheba, wakaishi
salama kila mtu chini ya mzabibu wake na
chini ya mtini wake.
26 Solomoni alikuwa na mabanda 4,000[f]
ya magari ya vita, na farasi 12,000.
27 Maafisa wa eneo hilo, kila mmoja
katika mwezi wake, walileta mahitaji kwa
ajili ya Mfalme Solomoni na wote waliokula
mezani mwa mfalme. Walihakikisha kuwa
hakuna chochote kilichopungua. 28 Pia
walileta sehemu walizopangiwa za shayiri
na majani kwa ajili ya farasi wavutao magari
na farasi wengine mahali palipostahili.

*Hekima Ya Solomoni*

29 Mungu akampa Solomoni hekima
na akili kubwa, pia ufahamu mpana
usiopimika kama mchanga ulioko pwani
ya bahari. 30 Hekima ya Solomoni ilikuwa
kubwa kuliko hekima ya watu wote wa
Mashariki na kubwa kuliko hekima yote
ya Misri. 31 Alikuwa na hekima kuliko kila
mwandishi, akiwemo Ethani Mwezrahi:
kuliko Hemani, Kalkoli na Darda, wana
wa Maholi. Umaarufu wake ukaenea kwa
mataifa yote yaliyomzunguka. 32 Akanena
mithali 3,000 na nyimbo zake zilikuwa
1,005. 33 Akaelezea maisha ya mimea
kuanzia mwerezi wa Lebanoni hadi hisopo
iotayo ukutani. Pia akafundisha kuhusu
wanyama na ndege, wanyama wenye
damu baridi, wakiwemo samaki. 34 Watu
wa mataifa yote wakaja kusikiliza hekima
ya Solomoni, waliotumwa na wafalme wote
wa ulimwengu, waliokuwa wamesikia juu
ya hekima yake.

*Maandalio Ya Ujenzi Wa Hekalu*

**(2 Nyakati 2:1-18)**

5 [g]Hiramu mfalme wa Tiro aliposikia kuwa
Solomoni ametiwa mafuta awe mfalme
mahali pa Daudi baba yake, akatuma
wajumbe kwa Solomoni, kwa sababu
Hiramu siku zote alikuwa na uhusiano
mzuri wa kirafiki na Daudi. 2 [h]Solomoni
akapeleka ujumbe huu kwa Hiramu:

3 [i]"Unajua kwamba kwa sababu ya
vita vilivyopiganwa dhidi ya baba
yangu Daudi kutoka pande zote,
hakuweza kujenga Hekalu kwa ajili
ya Jina la BWANA Mungu wake, hadi
BWANA alipowaweka adui zake chini
ya miguu yake. 4 Lakini sasa BWANA
Mungu wangu amenipa utulivu kila
upande hakuna adui wala maafa. 5 [j]Kwa
hiyo, ninakusudia kujenga Hekalu
kwa ajili ya Jina la BWANA, Mungu
wangu, kama BWANA alivyomwambia
baba yangu Daudi, wakati aliposema,
'Mwanao nitakayemweka kwenye kiti
cha ufalme mahali pako, ndiye atajenga
Hekalu kwa ajili ya Jina langu.'
6 [k]"Hivyo toa amri ili mierezi ya
Lebanoni ikatwe kwa ajili yangu.
Watu wangu watafanya kazi na watu
wako, nami nitawalipa watu wako
kwa ujira wowote utakaoupanga.
Unajua kwamba hatuna mtu yeyote
mwenye ustadi katika kukata miti
kama Wasidoni."

7 Hiramu aliposikia ujumbe wa Solomoni,
akafurahishwa sana akasema, "Ahimidiwe
BWANA leo, kwa kuwa amempa Daudi

---

[a]**4:22** Dan 6:2
[b]22 Kori 30 ni sawa na madebe 360.
[c]22 Kori 60 ni sawa na madebe 720.
[d]**4:23** Mit 4:16
[e]**4:24** Dan 9:25; Ay 20:5
[f]26 Waandishi wengine wanasema 40,000 (angalia 2Nya 9:25).
[g]**5:1** Ezr 6:14; Hag 1:14; Zek 8:9
[h]**5:2** 1Nya 3:19; Ezr 6:14; Mhu 12:11; Zek 4:6-10; Hag 1:2-15; 2:2-5
[i]**5:3** Ezr 6:6
[j]**5:5** 2Fal 25:28; 1Pet 3:12; 2Nya 16:9; Ezr 7:6, 28; Za 33:18; Isa 41:10
[k]**5:6** Ezr 4:9

mwana mwenye hekima kutawala juu ya
taifa hili kubwa.”
8 Hiramu akatuma neno kwa Solomoni:

“Nimepokea ujumbe ulionipelekea
na nitafanya yote unayohitaji katika
kukupatia magogo ya mierezi
na misunobari. 9 [a]Watu wangu
watayakokota kutoka Lebanoni hadi
kwenye bahari, nami nitayafunga
mafungu mafungu yaelee juu ya
maji hadi utakapoelekeza. Huko
nitayatenganisha, nawe utaweza
kuyachukua. Wewe utakidhi haja
yangu kwa kunipatia chakula kwa ajili
ya watu wa nyumbani mwangu.”

10 Kwa njia hii Hiramu akampa Solomoni
miti yote ya mierezi na magogo ya
misunobari kama alivyohitaji, 11 [b]naye
Solomoni akampa Hiramu kori 20,000[c]
za ngano kama chakula kwa ajili ya watu
wa nyumbani mwake, pamoja na mafuta
safi ya zeituni yaliyokamuliwa bathi
20,000.[d] Solomoni aliendelea kumfanyia
Hiramu hivyo mwaka baada ya mwaka.
12 [e]BWANA akampa Solomoni hekima, kama
alivyomwahidi. Palikuwepo na uhusiano
wa amani kati ya Hiramu na Solomoni, na
wote wawili wakafanya mkataba.
13 [f]Mfalme Solomoni akakusanya
wafanyakazi 30,000 kutoka Israeli yote.
14 [g]Akawapeleka Lebanoni kwa zamu za
watu 10,000 kwa mwezi, hivyo walikaa
Lebanoni kwa mwezi mmoja na miezi
miwili nyumbani. Adoniramu ndiye alikuwa
kiongozi wa shokoa. 15 Solomoni alikuwa na
wachukuzi wa mizigo 70,000 na wachonga
mawe 80,000 huko vilimani, 16 [h]pamoja na
wasimamizi 3,300 ambao walisimamia kazi
hiyo na kuwaongoza wafanyakazi. 17 [i]Kwa
amri ya mfalme walitoa kwenye machimbo
ya mawe, mawe makubwa, yaliyo bora kwa
kujengea msingi wa nyumba yaliyochongwa
kwa ajili ya Hekalu. 18 Mafundi wa
Solomoni, wa Hiramu na watu wa Gebali[j]
walikata na kuandaa mbao na mawe kwa
ajili ya ujenzi wa Hekalu.

### *Solomoni Ajenga Hekalu*

**(2 Nyakati 3)**

6 [k]Katika mwaka wa 480 baada ya
Waisraeli kutoka nchi ya Misri, katika
mwaka wa nne wa utawala wa Solomoni
katika Israeli, katika mwezi wa Zivu, ambao
ndio mwezi wa pili, alianza kujenga Hekalu
la BWANA.
2 Hekalu hilo Mfalme Solomoni alilojenga
kwa ajili ya BWANA lilikuwa na urefu wa
dhiraa sitini,[l] upana wa dhiraa ishirini[m]
na kimo cha dhiraa thelathini[n] kwenda
juu. 3 [o]Baraza ya mbele ya Hekalu ilienea
dhiraa ishirini kulingana na upana wa
Hekalu na kujitokeza dhiraa kumi mbele
ya Hekalu. 4 [p]Akatengeneza madirisha
membamba yenye vidirisha vidogo vya
juu katika Hekalu. 5 [q]Akafanyiza vyumba
vya pembeni kulizunguka Hekalu lote
vikishikamana na kuta za Hekalu na za
Patakatifu pa Patakatifu. 6 [r]Ghorofa ya chini
kabisa ilikuwa na upana wa dhiraa tano,[s] ya
kati ilikuwa dhiraa sita na ya tatu ilikuwa
dhiraa saba.[t] Kuzunguka ukuta wa nje wa
Hekalu akapunguza ukuta pande zote ili
boriti zisishikane kwenye kuta za Hekalu.
7 Katika kujenga Hekalu, yalitumika tu
mawe yaliyochongwa huko machimboni,
wala hakuna nyundo, patasi au chombo

[a]**5:9** Ezr 4:12
[b]**5:11** 1Fal 6:1; Yos 24:15; Za 119:46; Yn 1:9; Mt 10:32; Lk 12:8; Mdo 27:23; 2Nya 3:1, 2
[c]11 Kori 20,000 ni sawa na madebe 240,000.
[d]11 Bathi 20,000 ni sawa na madebe 200.
[e]**5:12** 2Nya 34:24-25; 36:16, 17; Yer 39:1; 2Fal 24:2
[f]**5:13** Ezr 1:1
[g]**5:14** Ezr 6:5; Dan 5:2; 1Nya 3:18; Hag 1:4
[h]**5:16** Ezr 3:10; 6:15; 4:15; 6:1-2
[i]**5:17** Ezr 6:1, 2; Mit 25:2
[j]18 Yaani Bubilo, mji wa zamani sana wa Ufoinike (kama kilomita 80 kaskazini mwa Beiruti).
[k]**6:1** Ezr 4:15; 5:17
[l]2 Dhiraa 60 ni sawa na mita 27.
[m]2 Dhiraa 20 ni sawa na mita 9.
[n]2 Dhiraa 30 ni sawa na mita 13.5.
[o]**6:3** Ezr 3:10; Hag 2:3
[p]**6:4** 1Fal 6:36; Ezr 7:20; Isa 60:6; Za 68:29
[q]**6:5** 1Nya 29:2; Yer 27:18-22; Ezr 5:14
[r]**6:6** Ezr 5:3
[s]6 Dhiraa 5 ni sawa na mita 2.25.
[t]6 Dhiraa saba ni sawa na mita 3.15.

kingine chochote cha chuma kilichosikika
sauti yake katika eneo la ujenzi wa Hekalu
wakati lilipokuwa likijengwa.
8 [a]Ingilio la ghorofa ya chini kabisa
lilikuwa upande wa kusini wa Hekalu,
ngazi ilielekea ghorofa ya kati na kutokea
hapo ilielekea hadi ghorofa ya tatu. 9 Basi
Solomoni akajenga Hekalu na kulikamilisha,
akiliweka paa za boriti na mbao za mierezi.
10 [b]Mfalme Solomoni akajenga vyumba vya
pembeni kuzunguka Hekalu lote. Kimo cha
kila kimoja kilikuwa dhiraa tano. Navyo
vilikuwa vimeunganishwa na Hekalu kwa
boriti za mierezi.
11 [c]Neno la BWANA likamjia Solomoni
kusema: 12 [d]"Kwa habari ya Hekalu hili
unalojenga, kama ukifuata amri zangu,
ukatunza masharti yangu na kushika
maagizo yangu yote na kuyatii, kwa kupitia
wewe nitatimiza ahadi niliyomwahidi Daudi
baba yako. 13 [e]Nami nitakaa miongoni mwa
Waisraeli, nami sitawaacha watu wangu
Israeli."
14 [f]Basi Solomoni akajenga Hekalu na
kulikamilisha. 15 [g]Akazifunika kuta zake za
ndani kwa mbao za mierezi, akizipigilia
ukutani kuanzia sakafuni mwa Hekalu hadi
kwenye dari na kufunika sakafu ya Hekalu
kwa mbao za misunobari. 16 [h]Akagawa
dhiraa ishirini sehemu ya nyuma ya Hekalu
kwa mbao za mierezi kuanzia kwenye
sakafu hadi darini ili kufanya sehemu
takatifu ya ndani, yaani Patakatifu pa
Patakatifu. 17 [i]Ukumbi mkubwa uliokuwa
mbele ya chumba hiki ndio ulikuwa na
urefu wa dhiraa arobaini.[j] 18 [k]Hekalu ndani
ilikuwa ya mierezi iliyonakshiwa mifano ya
maboga na maua yaliyochanua. Kila kitu
kilikuwa cha mwerezi, hakuna jiwe ambalo
lilionekana.
19 [l]Ndani ya Hekalu akatengeneza sehemu
takatifu ya ndani, kwa ajili ya kuweka
Sanduku la Agano la BWANA. 20 [m]Sehemu
takatifu ya ndani ilikuwa na upana, urefu
na kimo cha dhiraa ishirini ndani kwa
ndani. Akaifunika ndani kwa dhahabu safi,
pia akaifunika madhabahu ya mierezi vivyo
hivyo. 21 [n]Solomoni akaifunika sehemu ya
ndani ya Hekalu kwa dhahabu safi, naye
akaitandaza mikufu ya dhahabu kutoka
upande moja hadi ule mwingine mbele
ya Patakatifu pa Patakatifu, ambako
palifunikwa kwa dhahabu. 22 [o]Basi akafunika
sehemu yote ya ndani kwa dhahabu. Pia
akafunika madhabahu yale yaliyokuwa
ndani ya Patakatifu pa Patakatifu kwa
dhahabu.
23 Katika Patakatifu pa Patakatifu
akatengeneza makerubi wawili kwa
mzeituni, kila moja likiwa na dhiraa kumi[p]
kwenda juu. 24 Bawa moja la kerubi wa
kwanza lilikuwa na urefu wa dhiraa tano
na bawa jingine dhiraa tano, hivyo urefu
kutoka ncha ya bawa moja hadi ncha ya
bawa jingine ulikuwa dhiraa kumi. 25 Kerubi
wa pili alikuwa na urefu wa dhiraa kumi
pia, hivyo makerubi hao wawili walifanana
kwa vipimo na kwa umbo. 26 Kimo cha kila
kerubi kilikuwa dhiraa kumi. 27 Aliwaweka
makerubi hao ndani ya Patakatifu pa
Patakatifu pa Hekalu, mabawa yake yakiwa
yamekunjuliwa. Bawa la kerubi mmoja
liligusa ukuta mmoja, wakati bawa la yule
mwingine liligusa ukuta mwingine, nayo
mabawa yao mengine yaligusana katikati
ya chumba. 28 Akafunika wale makerubi
kwa dhahabu.
29 Juu ya kuta zote zilizozunguka Hekalu,
za vyumba vya ndani na vya nje, zilipambwa
kwa nakshi zilizokatwa za makerubi, miti

[a]**6:8** 1Sam 9:10
[b]**6:10** Ezr 7:23; Yer 29:7; Law 1:9; Mwa 8:21; 1Tim 2:1-2
[c]**6:11** Kum 21:22-23; Es 2:23; Ezr 7:26; Dan 2:5
[d]**6:12** Kut 20:24; Kum 12:11; 1Fal 9:3; 2Nya 7:16; Za 132:13
[e]**6:13** Ay 5:12; Ezr 4:9; Za 9:16; 1Kor 3:19
[f]**6:14** Ezr 5:1; 7:1; Neh 2:1; Ezr 4:24
[g]**6:15** Zek 4:9
[h]**6:16** 1Fal 8:63; 2Nya 7:15; Yn 10:22
[i]**6:17** 2Sam 6:13; 1Nya 16:1-3; 2Nya 29:21; Hes 7:2-3; Ezr 8:25
[j]17 Dhiraa 40 ni sawa na mita 18.
[k]**6:18** 1Nya 24:1; 23:6; Hes 3:6-9; 8:9-11
[l]**6:19** Kut 12:11; Hes 28:16
[m]**6:20** 2Nya 30:15-17; 35:11; Kut 12:25; 2Nya 29:34
[n]**6:21** Kut 12:48; Za 93:5
[o]**6:22** Kut 12:17; Mit 21:1; Ezr 1:1
[p]23 Dhiraa 10 ni sawa na mita 4.5.

ya mitende na maua yaliyochanua. 30 Pia
alifunika sakafu zote za vyumba vya ndani
na vya nje vya Hekalu kwa dhahabu.

31 Kwa ingilio la Patakatifu pa Patakatifu
akatengeneza milango ya mbao za mzeituni,
zikiwa na miimo na vizingiti vyenye umbo
la pembe tano. 32 Juu ya milango miwili ya
mbao za mzeituni alinakshi makerubi, miti
ya mitende pamoja na maua yaliyochanua
na kufunika makerubi na miti ya mitende
kwa dhahabu iliyofuliwa. 33 Kwa njia iyo
hiyo akatengeneza miimo yenye pande
nne ya miti ya mizeituni, kwa ajili ya
ingilio la ukumbi mkubwa. 34 Kulikuwa
na milango miwili iliyoweza kukunjuka
iliyotengenezwa kwa mbao za msunobari
na kila mmoja ulikuwa na bawaba ambazo
zingeuwezesha kujikunja kila kipande juu
ya kingine. 35 Akanakshi makerubi, miti ya
mitende na maua yaliyochanua juu yake
na kufunika kwa dhahabu iliyonyooshwa
vizuri juu ya michoro.

36 Tena akajenga ua wa ndani safu tatu
za mawe yaliyochongwa na safu moja ya
boriti za mierezi zilizorembwa.

37 Msingi wa Hekalu la Bwana uliwekwa
katika mwaka wa nne, katika mwezi wa
Zivu, ndio mwezi wa tano. 38 Katika
mwaka wa kumi na moja, mwezi wa Buli,
ndio mwezi wa nane, Hekalu lilikamilika
katika hatua zake zote kwa kufuatana na
maelekezo yake Solomoni. Alilijenga kwa
miaka saba.

### *Solomoni Ajenga Jumba Lake La Kifalme*

7 [a]Ilimchukua Solomoni miaka kumi na
mitatu kukamilisha ujenzi wa Jumba
lake la kifalme. 2 [b]Alijenga Jumba la Kifalme
la Msitu wa Lebanoni, urefu wake ulikuwa
dhiraa 100,[c] upana wake dhiraa hamsini na
kimo chake dhiraa thelathini,[d] likiwa na
safu nne za nguzo za mierezi zikishikilia
boriti za mierezi zilizorembwa. 3 Ilipauliwa
kwa mierezi juu ya boriti zile zilizolala juu
ya nguzo arobaini na tano, kumi na tano
kwa kila safu. 4 Madirisha yake yaliwekwa
juu kwa safu tatu, yakielekeana. 5 Milango
yote ilikuwa na miimo ya mstatili, ilikuwa
upande wa mbele katika safu tatu,
ikielekeana.

6 [e]Akajenga ukumbi wa nguzo, ambao
urefu wake ulikuwa dhiraa hamsini[f] na
upana wake dhiraa thelathini. Mbele ya
jengo hilo kulikuwepo baraza. Mbele
ya baraza kulikuwepo na nguzo na paa
lililoning'inia.

7 [g]Akajenga ukumbi wa kiti cha enzi,
Ukumbi wa Hukumu, mahali ambapo
angelitolea hukumu, akaufunika kwa
mierezi kutoka sakafuni hadi darini.
8 Kwenye jumba la kifalme ambamo
angeliishi, aliiweka nyuma zaidi, ikiwa na
mjengo wa aina moja na hiyo nyingine.
Pia Solomoni akajenga jumba la kifalme
linalofanana na huo ukumbi mkubwa kwa
ajili ya binti Farao, aliyekuwa amemwoa.

9 [h]Ujenzi huu wote, kuanzia nje mpaka
kwenye ua mkuu na kuanzia kwenye msingi
hadi upenuni, ulifanywa kwa mawe ya ubora
wa hali ya juu yaliyokuwa yamechongwa
kwa vipimo na kusawazishwa kwa
msumeno nyuso zake za ndani na za nje.
10 [i]Misingi iliwekwa kwa mawe makubwa
yaliyo bora, yenye urefu wa dhiraa kumi[j]
na mengine yenye urefu wa dhiraa nane[k]
11 Sehemu za juu kulikuwepo na mawe
yenye ubora wa hali ya juu, yaliyokatwa
kwa vipimo na boriti za mierezi. 12 [l]Ule ua
mkuu ulizungukwa na ukuta wa safu tatu za
mawe yaliyochongwa na safu moja ya boriti
za mierezi zilizorembwa, kama ulivyokuwa
ua wa ndani wa Hekalu la Bwana na baraza
yake.

---

[a]**7:1** Ezr 4:7; Neh 2:1; 1Nya 6:14
[b]**7:2** 1Fal 2:35; Neh 11:11
[c]2 Dhiraa 100 ni sawa na mita 45.
[d]2 Dhiraa 30 ni sawa na mita 13.5.
[e]**7:6** Neh 12:36; Ezr 5:5; Isa 41:20; Mwa 32:28; Neh 1:10-11
[f]6 Dhiraa 50 ni sawa na mita 22.5.
[g]**7:7** Ezr 8:1; 2:43
[h]**7:9** Neh 2:8
[i]**7:10** Kum 33:10; Neh 8:1-8; 2Tim 4:2; 1Sam 7:3; 2Nya 12:14; Za 10:18; 119:45; Mal 2:7
[j]10 Dhiraa 10 ni sawa na mita 4.5.
[k]10 Dhiraa nane ni sawa na mita 3.6.
[l]**7:12** Dan 2:37; Ezr 4:10

*Samani Za Hekalu*

**(2 Nyakati 4)**

13 Mfalme Solomoni akatuma watu Tiro
kumleta Hiramu, 14 [a]ambaye mama yake
alikuwa mjane kutoka kabila la Naftali na
baba yake alikuwa mtu wa Tiro tena fundi
wa shaba. Hiramu alikuwa na ustadi wa hali
ya juu na mzoefu katika aina zote za kazi
ya shaba. Alikuja kwa Mfalme Solomoni
na kufanya kazi zake zote alizopangiwa.

15 [b]Hiramu akasubu nguzo mbili za shaba,
kila moja ikiwa na urefu wa dhiraa kumi
na nane,[c] kila nguzo ikiwa na mzingo wa
dhiraa kumi na mbili[d] kwa mstari. 16 [e]Pia
alitengeneza mataji mawili ya shaba ya
kusubu ili kuyaweka juu ya hizo nguzo;
kila taji lilikuwa na kimo cha dhiraa
tano[f] kwenda juu. 17 [g]Wavu wa mikufu
iliyosokotewa kwenye zile taji juu ya zile
nguzo, saba kwa kila taji. 18 Akatengeneza
makomamanga katika safu mbili kuzunguka
kila wavu kuremba mataji yaliyo juu ya
nguzo. Alifanya hivyo kwa kila nguzo.
19 [h]Mataji yaliyokuwa juu ya nguzo
kwenye baraza, yalikuwa katika umbo la
yungiyungi, kimo chake ni dhiraa nne[i]
20 [j]Juu ya mataji ya zile nguzo mbili, juu
ya ile sehemu yenye umbo kama bakuli,
karibu na ule wavu, kulikuwa na yale
makomamanga 200 katika safu kuzunguka
pande zote. 21 [k]Hiramu akasimamisha nguzo
kwenye baraza ya Hekalu. Nguzo ya upande
wa kusini akaiita Yakini,[l] na ile ya upande
wa kaskazini Boazi.[m] 22 Mataji yaliyokuwa
juu yalikuwa na umbo la yungiyungi. Hivyo
kazi ya nguzo ikakamilika.

23 [n]Hiramu akasubu Bahari ya chuma,
yenye umbo la mviringo, ya dhiraa kumi
kutoka ukingo hadi ukingo na kimo cha
dhiraa tano. Mzunguko wake ulikuwa
dhiraa thelathini. 24 [o]Chini ya ukingo,
ilizungukwa na maboga, kumi kwenye kila
dhiraa moja. Maboga yalikuwa yamesubiwa
katika safu mbili ili kuwa kitu kimoja na
hiyo bahari.

25 [p]Bahari iliwekwa juu ya mafahali kumi
na wawili, watatu wakielekea kaskazini,
watatu wakielekea magharibi, watatu
wakielekea kusini na watatu wakielekea
mashariki. Bahari iliwekwa juu yao
na sehemu zao za nyuma zilielekeana.
26 [q]Ilikuwa na unene wa nyanda nne[r]
na ukingo wake ulifanana na ukingo
wa kikombe, kama ua la yungiyungi
iliyochanua. Iliweza kuchukua bathi 2,000.[s]

27 [t]Pia akatengeneza vitako kumi vya
shaba vinavyoweza kuhamishika, kila
kimoja kilikuwa na urefu wa dhiraa
nne, upana dhiraa nne na kimo chake
dhiraa tatu[u] 28 [v]Hivi ndivyo vile vitako
vilivyotengenezwa: Vilikuwa na mbao za
pembeni zilizoshikamanishwa na mihimili.
29 Juu ya mbao kati ya hiyo mihimili
kulikuwa na simba, mafahali na makerubi,
pia kwenye mihimili yake. Juu na chini ya
simba na mafahali kulikuwa kumesokotewa
taji za kufuliwa. 30 Kila kitako kilikuwa na
magurudumu manne ya shaba, na vyuma
vya katikati vya kuyazungusha hayo
magurudumu na kila kimoja kilikuwa
na sinia kwenye vishikizo vinne vya taji
iliyosubiwa kila upande. 31 Ndani ya kitako
kulikuwa na nafasi ya wazi iliyokuwa

---

[a]**7:14** Es 1:14
[b]**7:15** Kum 12:5; 1Nya 29:6; 2Nya 6:2; Za 135:21
[c]15 Dhiraa 18 ni sawa na mita 8.1.
[d]15 Dhiraa 12 ni sawa na mita 5.4.
[e]**7:16** Kut 3:22; Ezr 8:25; Zek 6:10; 1Nya 29:6
[f]16 Dhiraa 5 ni sawa na mita 2.25.
[g]**7:17** 2Fal 3:5; Hes 15:5-12
[h]**7:19** Ezr 5:14; Yer 27:22
[i]19 Dhiraa nne ni sawa na mita 1.8.
[j]**7:20** Ezr 6:4; 1Kor 4:1-2
[k]**7:21** Ezr 4:16-20; 5:3-6
[l]21 Yakini maana yake Mungu atafanya imara.
[m]21 Boazi maana yake Ndani ya Mungu kuna nguvu.
[n]**7:23** Ezr 6:10; Isa 60:12; Yer 12:14; Za 68:29; 1Tim 2:1-2
[o]**7:24** Ezr 4:13; 8:36
[p]**7:25** Kut 18:21-26; 16:18; Za 19:7; Kol 1:28; Kum 16:18; 2Nya 17:7; Mal 2:7; Mt 13:52
[q]**7:26** Eze 6:11
[r]26 Nyanda nne ni sawa na sentimita 32. Nyanda moja ni sawa na upana wa kiganja kimoja, ambacho ni sawasawa na sentimita 8.
[s]26 Bathi 2,000 ni sawa na lita 40,000.
[t]**7:27** Ezr 6:22; 1Nya 29:12; Neh 2:12; 2Kor 8:16; Flp 4:10; Mit 16:7
[u]27 Dhiraa 3 ni sawa na mita 1.35.
[v]**7:28** 2Fal 25:28; Ezr 5:5; 9:9; Neh 1:11

na umbile la mviringo lenye kina cha
dhiraa moja.[a] Nafasi hii ya wazi ilikuwa
ya mviringo, pamoja na kitako chake
ilikuwa dhiraa moja na nusu.[b] Kuzunguka
huo mdomo wake kulitiwa nakshi. Papi za
vitako zilikuwa mraba na si za mviringo.
32 Magurudumu manne yalikuwa chini
ya papi, na vyuma vya katikati vya
kuzungushia magurudumu hayo vilikuwa
vimeunganishwa kwenye kitako. Kipenyo
cha kila gurudumu kilikuwa dhiraa moja na
nusu. 33 Magurudumu yalitengenezwa kama
ya magari ya vita ya kukokotwa, vyuma
vya katikati vya magurudumu, duara zake,
matindi yake na vikombe vyake vyote
vilikuwa vya kusubu.

34 Kila kitako kilikuwa na mikono minne,
moja kwenye kila pembe, ukitokeza kutoka
kwenye kitako. 35 Juu ya kitako kulikuwepo
na utepe wa mviringo wenye kina cha nusu
dhiraa. Vishikio na papi vilishikamana
upande wa juu wa kitako. 36 Alitia nakshi
za makerubi, simba na miti ya mitende juu
ya uso wa vishikio na juu ya papi, katika
kila nafasi iliyopatikana, pamoja na mataji
yaliyosokotwa kuzunguka pande zote.
37 Hivi ndivyo Hiramu alivyotengeneza vile
vitako kumi. Vyote vilikuwa vya kusubu
kwenye kalibu za kufanana kwa vipimo na
kwa umbo.

38 Kisha akatengeneza masinia kumi ya
shaba, kila moja likiwa na ujazo wa bathi
arobaini,[c] yakiwa na kipenyo cha dhiraa
nne[d] kila sinia moja kwa kila kimoja ya
vile vitako kumi. 39 Aliweka vitako vitano
upande wa kusini wa Hekalu na vingine
vitano upande wa kaskazini. Akaweka ile
bahari upande wa kusini, katika pembe
ya kusini ya Hekalu. 40 Pia akatengeneza
masinia, masepetu na mabakuli ya
kunyunyizia.

Kwa hiyo Huramu akakamilisha kazi zote katika Hekalu la Bwana kama vile Mfalme Solomoni alikuwa amemwagiza, yaani:

41 nguzo mbili;
mataji mawili yenye umbo la bakuli
juu ya hizo nguzo;
nyavu mbili za kupamba hayo mataji
mawili yenye umbo la bakuli juu
ya hizo nguzo;
42 makomamanga 400 kwa ajili ya
hizo nyavu mbili (safu mbili za
makomamanga kwa kila wavu,
yakipamba hayo mataji mawili
yenye umbo la bakuli juu ya hizo
nguzo);
43 vitako kumi pamoja na masinia yake
kumi;
44 ile Bahari ya chuma na yale mafahali
kumi na wawili chini yake;
45 masufuria, masepetu na mabakuli ya
kunyunyizia.

Vyombo hivi vyote ambavyo Huramu
alimtengenezea Mfalme Solomoni kwa
ajili ya Hekalu la Bwana vilikuwa vya
shaba iliyong'arishwa. 46 Mfalme akaamuru
wavisubu katika kalibu ya udongo wa
mfinyanzi katika uwanda wa Yordani ulio
kati ya Sukothi na Sarethani. 47 Solomoni
akaviacha vitu hivi vyote bila kupima uzani
wake, kwa sababu vilikuwa vingi sana hivi
kwamba uzito wa shaba haungekadirika.

48 Solomoni pia akatengeneza samani
zote zilizokuwa ndani ya Hekalu la Bwana:

madhabahu ya dhahabu;
meza ya dhahabu za kuweka mikate
ya Wonyesho;
49 vinara vya taa vya dhahabu safi
(vitano upande wa kuume na
vitano upande wa kushoto, mbele
ya Patakatifu pa Patakatifu);
kazi ya maua ya dhahabu na taa na
makoleo;
50 masinia ya dhahabu safi, mikasi ya
kusawazishia tambi, mabakuli ya
kunyunyizia, vyano na vyetezo;
na bawaba za dhahabu kwa ajili
ya milango ya chumba cha
ndani sana, yaani Patakatifu pa
Patakatifu, na pia kwa ajili ya
milango ya ukumbi mkuu wa
Hekalu.

51 Hivyo Mfalme Solomoni alipomaliza

[a]31 Dhiraa moja ni sawa na sentimita 45.
[b]31 Dhiraa moja na nusu ni sawa na sentimita 67.5.
[c]38 Bathi 40 ni sawa na lita 800.
[d]38 Dhiraa nne ni sawa na mita 1.8.

kazi ya Hekalu la Bwana, akaviingiza
ndani vile vitu ambavyo Daudi baba yake
alikuwa ameviweka wakfu: yaani fedha,
dhahabu na samani; kisha akaviweka katika
hazina za Hekalu la Bwana.

*Sanduku La Agano Laletwa Hekaluni*

**(2 Nyakati 5)**

8 [a]Kisha Mfalme Solomoni akawaita mbele
zake huko Yerusalemu wazee wa Israeli,
viongozi wote wa makabila na wakuu wa
jamaa za Waisraeli, ili walilete Sanduku
la Agano la Bwana kutoka Sayuni, Mji
wa Daudi. 2 [b]Wanaume wote wa Israeli
wakakusanyika kwa Mfalme Solomoni
wakati wa sikukuu ya mwezi wa Ethanimu,
ndio mwezi wa saba.

3 [c]Wazee wote wa Israeli walipofika,
makuhani wakajitwika Sanduku la Agano,
4 [d]nao wakalipandisha Sanduku la Bwana,
na Hema la Kukutania pamoja na vyombo
vyote vitakatifu vilivyokuwa ndani yake.
Makuhani na Walawi wakavibeba, 5 naye
Mfalme Solomoni na kusanyiko lote
la Israeli waliokusanyika kumzunguka
walikuwa mbele ya hilo Sanduku, nao
wakatoa dhabihu nyingi za kondoo na
ng’ombe ambao idadi yao haikuwezekana
kuandikwa au kuhesabiwa.

6 [e]Makuhani wakalileta Sanduku la Agano
la Bwana hadi mahali pake ndani ya sehemu
takatifu ndani ya Hekalu, yaani Patakatifu
pa Patakatifu, na kuliweka chini ya mabawa
ya makerubi. 7 Makerubi yalitandaza
mabawa yao juu ya mahali pa Sanduku
la Agano na kutia kivuli Sanduku pamoja
na mipiko yake ya kubebea. 8 Mipiko hiyo
ilikuwa mirefu sana kiasi kwamba ncha zake
zilionekana kutoka Mahali Patakatifu mbele
ya Patakatifu pa Patakatifu, lakini sio nje
ya Mahali Patakatifu. Hiyo mipiko ipo hata
leo. 9 Ndani ya Sanduku hapakuwepo kitu
kingine chochote isipokuwa zile mbao mbili
za mawe ambazo Mose alikuwa ameziweka
ndani yake huko Horebu, mahali ambapo
Bwana alifanya Agano na Waisraeli baada
ya kutoka Misri.

10 Makuhani walipoondoka katika
Mahali Patakatifu, wingu likajaza Hekalu
la Bwana. 11 Nao makuhani hawakuweza
kufanya huduma yao kwa sababu ya lile
wingu, kwa kuwa utukufu wa Bwana
ulijaza Hekalu lake.

12 Ndipo Solomoni akasema, “Bwana
alisema kwamba ataishi katika giza nene;
13 [f]naam, hakika nimekujengea Hekalu zuri
sana, mahali pako pa kuishi milele.”

*Hotuba Ya Solomoni*

**(2 Nyakati 6:3-11)**

14 Kusanyiko lote la Israeli lilipokuwa
limesimama hapo, mfalme akageuka na
kuwabariki. 15 [g]Kisha akasema:

“Ahimidiwe Bwana, Mungu
wa Israeli, ambaye kwa mkono
wake mwenyewe ametimiza lile
alilomwahidi Daudi baba yangu kwa
kinywa chake mwenyewe. Kwa kuwa
alisema, 16 ‘Tangu siku niliyowatoa
watu wangu Israeli kutoka Misri,
sikuchagua mji katika kabila lolote
la Israeli ili Hekalu lijengwe humo ili
Jina langu lipate kuwamo humo, bali
nimemchagua Daudi kuwatawala watu
wangu Israeli.’

17 [h]“Ilikuwa moyoni mwa Daudi baba
yangu kujenga Hekalu kwa ajili ya Jina
la Bwana, Mungu wa Israeli. 18 [i]Lakini
Bwana akamwambia Daudi baba
yangu, ‘Kwa sababu ilikuwa moyoni
mwako kujenga Hekalu kwa ajili ya
Jina langu, ulifanya vyema kuwa na
jambo hili moyoni mwako. 19 Hata
hivyo, sio wewe utakayenijengea
hekalu, bali mwanao, ambaye ni
nyama yako na damu yako mwenyewe,
yeye ndiye atakayejenga Hekalu kwa
ajili ya Jina langu.’

[a]**8:1** Ezr 7:7
[b]**8:2** 1Nya 3:22
[c]**8:3** 1Nya 3:22; Ezr 2:3
[d]**8:4** Ezr 2:6
[e]**8:6** Ezr 2:15; Neh 7:20
[f]**8:13** Ezr 2:13
[g]**8:15** Ezr 2:40; 7:7; Mdo 16:13; 20:28; Za 137:1; Mit 27:23; Ebr 13:17; Ezr 7:7; Hes 8:1
[h]**8:17** Ezr 2:43
[i]**8:18** Ezr 5:5; 7:28; Neh 8:7; Rum 8:28; Mit 3:6; Law 10:10-11; 2Nya 30:22

[20] [a]"BWANA ametimiza ahadi aliyoiweka: Nimeingia mahali pa Daudi baba yangu na sasa ninakikalia kiti cha ufalme cha Israeli, kama vile BWANA alivyoahidi, nami nimejenga Hekalu kwa ajili ya Jina la BWANA, Mungu wa Israeli. [21] [bc]Nimetenga nafasi humo kwa ajili ya Sanduku la Agano, ambamo ndani yake kuna lile Agano la BWANA alilofanya na baba zetu wakati alipowatoa Misri."

*Maombi Ya Solomoni Ya Kuweka Hekalu Wakfu*

**(2 Nyakati 6:12-42)**

[22] [d]Kisha Solomoni akasimama mbele ya madhabahu ya BWANA machoni pa kusanyiko lote la Israeli, akakunjua mikono yake kuelekea mbinguni [23] [e]na kusema:

"Ee BWANA, Mungu wa Israeli, hakuna Mungu kama wewe juu mbinguni wala chini duniani, wewe unayetunza Agano lako la upendo na watumishi wanaodumu katika njia yako kwa moyo wote. [24] Umetimiza ahadi yako kwa mtumishi wako Daudi baba yangu, kwa kinywa chako uliahidi na kwa mkono wako umetimiza, kama ilivyo leo.

[25] [f]"Sasa BWANA, Mungu wa Israeli, mtimizie mtumishi wako Daudi baba yangu ahadi zako ulizomwahidi uliposema, 'Kamwe hutakosa kuwa na mtu atakayeketi mbele zangu kwenye kiti cha ufalme cha Israeli, kama wanao wakiangalia yote wayafanyayo kuenenda mbele zangu kama vile ulivyofanya.' [26] Sasa, Ee Mungu wa Israeli, acha neno lako lile ulilomwahidi mtumishi wako Daudi baba yangu litimie.

[27] "Lakini kweli, je, Mungu atafanya makao duniani? Mbingu, hata mbingu zilizo juu sana, haziwezi kukutosha wewe. Sembuse Hekalu hili nililojenga! [28] [g]Hata hivyo sikiliza dua ya mtumishi wako na maombi yake kwa huruma, Ee BWANA Mungu wangu. Sikia kilio na dua ambayo mtumishi wako anaomba mbele zako siku hii ya leo. [29] [h]Macho yako na yafumbuke kuelekea Hekalu hili usiku na mchana, mahali hapa ambapo ulisema, 'Jina langu litakuwako humo,' ili kwamba upate kusikia maombi ambayo mtumishi wako ataomba kuelekea mahali hapa. [30] Usikie maombi ya mtumishi wako na ya watu wako Israeli wakati wanapoomba kuelekea mahali hapa. Sikia kutoka mbinguni, mahali pa makao yako na usikiapo, samehe.

[31] [i]"Mtu anapomkosea jirani yake na akatakiwa kuapa, akija na kuapa mbele ya madhabahu yako ndani ya Hekalu hili, [32] [j]basi, sikia kutoka mbinguni na ukatende. Hukumu kati ya watumishi wako, ukimhukumu yule mwenye hatia na kuleta juu ya kichwa chake yale aliyoyatenda. Umtangazie mwenye haki kwamba hana hatia, hivyo ukathibitishe kuwa haki kwake.

[33] [k]"Wakati watu wako Israeli watakapokuwa wameshindwa na adui kwa sababu ya dhambi walizofanya dhidi yako, watakapokugeukia na kulikiri jina lako, wakiomba na kufanya dua kwako katika Hekalu hili, [34] basi usikie kutoka mbinguni, ukasamehe dhambi ya watu wako Israeli na kuwarudisha katika nchi uliyowapa baba zao.

[35] [l]"Wakati mbingu zitakapokuwa

[a]**8:20** 1Nya 9:2; Ezr 2:43
[b]**8:21** 2Nya 9:2; Ezr 2:43
[c]**8:21** 2Nya 20:3; Za 27:11; Law 16:29; Za 5:8; 2Nya 20:3; Law 16:29; Isa 58:3-5
[d]**8:22** Neh 2:9; Yer 41:16; 2Nya 15:2; 1Kor 9:15; 1Nya 28:9; Ezr 7:6-9; Za 33:18-19; Isa 3:10; Rum 8:28; 1Pet 3:12; Za 34:16; 2Nya 15:2
[e]**8:23** 2Nya 33:13; Kum 4:29; Mdo 14:23; 1Nya 5:20; Isa 19:22; Yer 29:12-13
[f]**8:25** Ezr 7:15-16
[g]**8:28** Kum 33:8; Law 21:6; 22:2-3; 2Nya 24:14; Hes 4:4; Isa 52:11; 1Nya 23:28
[h]**8:29** 1Nya 26:20-26; Lk 12:38-39
[i]**8:31** Ay 5:19-24; Isa 41:10-14; Ezr 7:6-7, 28
[j]**8:32** Mwa 40:13; Neh 2:11; Isa 56:6; 14:1
[k]**8:33** Neh 3:3, 21-24
[l]**8:35** Ezr 6:17

zimefungwa kusiwe na mvua kwa
sababu watu wako wametenda dhambi
dhidi yako, watakapoomba kuelekea
mahali hapa na kulikiri jina lako nao
wakageuka kutoka dhambi zao kwa
sababu umewaadhibu, 36 [a]basi usikie
kutoka mbinguni na usamehe dhambi
ya watumishi wako, watu wako Israeli.
Wafundishe njia sahihi ya kuishi na
ukanyeshe mvua juu ya nchi uliyowapa
watu wako kuwa urithi.

37 "Wakati njaa au tauni vikija juu ya
nchi, au koga au kawa, nzige au panzi,
au wakati adui atakapowazingira
katika mji wao wowote, maafa ya
namna yoyote au ugonjwa wowote
unaoweza kuwajia, 38 wakati dua
au maombi yatakapofanywa na
mmojawapo wa watu wako Israeli,
kila mmoja akitambua taabu za moyo
wake mwenyewe, naye akainyoosha
mikono yake kuelekea Hekalu hili:
39 basi usikie kutoka mbinguni, katika
makao yako. Usamehe na utende,
umpe kila mtu kulingana na matendo
yake, kwa kuwa unaujua moyo wake
(kwa kuwa ni wewe peke yako ujuaye
mioyo ya watu wote), 40 ili wakuogope
kwa wakati wote watakaoishi katika
nchi uliyowapa baba zetu.

41 "Kwa habari ya mgeni ambaye
si miongoni mwa watu wako Israeli,
lakini amekuja kutoka nchi ya mbali
kwa sababu ya jina lako, 42 kwa maana
watu watasikia juu ya Jina lako kuu
na juu ya mkono wako wenye nguvu
na mkono wako ulionyooshwa,
atakapokuja na kuomba kuelekea
Hekalu hili, 43 basi na usikie kutoka
mbinguni, mahali pa makao yako,
ukafanye lolote ambalo mgeni huyo
anakuomba, ili mataifa yote ya dunia
wapate kujua jina lako na wakuogope
kama wafanyavyo watu wako Israeli
nao wapate pia kujua kwamba nyumba
hii niliyoijenga imeitwa kwa Jina lako.

44 "Wakati watu wako
watakapokwenda vitani dhidi ya
adui zao, popote utakapowapeleka,
wakati watakapoomba kwa Bwana
kuelekea mji ambao umeuchagua, na
Hekalu nililolijenga kwa ajili ya Jina
lako, 45 basi usikie dua na maombi yao
kutoka mbinguni, ukawatetee haki
yao.

46 "Watakapotenda dhambi dhidi
yako, kwa kuwa hakuna mtu yeyote
ambaye hatendi dhambi, nawe
ukachukizwa nao na kuwakabidhi kwa
adui, ambaye atawachukua utumwani
katika nchi yake mwenyewe, mbali au
karibu; 47 na kama watabadilika mioyo
yao katika nchi wanakoshikiliwa
mateka, nao wakatubu na kukulilia
katika nchi ya wale waliowashinda
na kusema, 'Tumetenda dhambi,
tumefanya makosa, tumetenda uovu';
48 kama wakikugeukia kwa moyo wao
wote na nafsi zao katika nchi ya adui
zao ambao waliwachukua mateka,
wakakuomba kuelekea nchi uliyowapa
baba zao, kuelekea mji uliouchagua
na Hekalu nililolijenga kwa ajili ya
Jina lako; 49 basi kutoka mbinguni,
mahali pa makao yako, usikie dua yao
na maombi yao na kuitetea haki yao.
50 Uwasamehe watu wako, waliotenda
dhambi dhidi yako; uwasamehe
makosa yote waliyoyatenda dhidi
yako, ukawafanye wale waliowashinda
kuwaonea huruma; 51 kwa maana ni
watu wako na urithi wako, uliowatoa
Misri, kutoka kwenye lile tanuru la
kuyeyushia chuma.

52 "Macho yako na yafumbuke juu
ya ombi la mtumishi wako na ombi la
watu wako Israeli, nawe uwasikilize
wakati wowote wanapokulilia. 53 Kwa
maana uliwachagua wao kutoka
mataifa yote ya ulimwengu kuwa urithi
wako mwenyewe, kama ulivyotangaza
kupitia mtumishi wako Mose wakati
wewe, Ee Bwana Mwenyezi,
ulipowatoa baba zetu kutoka Misri."

54 Wakati Solomoni alipomaliza dua hizi
zote na maombi kwa Bwana, akainuka
kutoka mbele ya madhabahu ya Bwana,
mahali alipokuwa amepiga magoti, mikono

[a]**8:36** Ezr 7:21-24; Zek 8:1-23; Es 9:3

yake ikawa imekunjuliwa kuelekea juu
mbinguni. 55 Akasimama na kubariki
kusanyiko lote la Israeli kwa sauti kubwa
akisema:

56 "Ahimidiwe BWANA, aliyewapa
pumziko watu wake Israeli kama vile
alivyokuwa ameahidi. Hakuna hata
neno moja lililopunguka kati ya ahadi
zote nzuri alizozitoa kupitia mtumishi
wake Mose. 57 BWANA Mungu wetu na
awe pamoja nasi kama alivyokuwa
na baba zetu, kamwe asituache wala
kutukataa. 58 Yeye na aielekeze mioyo
yetu kwake, ili tutembee katika njia
zake zote na kuzishika amri na maagizo
na masharti aliyowapa baba zetu.
59 Nami maneno yangu haya, ambayo
nimeyaomba mbele za BWANA, yawe
karibu na BWANA Mungu wetu usiku
na mchana, ili kwamba atetee shauri
la mtumishi wake na la watu wake
Israeli kulingana na hitaji lao la kila
siku, 60 ili kwamba mataifa yote ya
dunia wajue kwamba BWANA ndiye
Mungu na kwamba hakuna mwingine.
61 Lakini ni lazima mwiweke mioyo
yenu kikamilifu kwa BWANA Mungu
wetu, kuishi kwa maagizo yake na kutii
amri zake, kama ilivyo wakati huu."

*Kuwekwa Wakfu Hekalu*

**(2 Nyakati 7:4-10)**

62 Kisha mfalme na Israeli wote pamoja
naye wakatoa dhabihu mbele za BWANA.
63 Solomoni akatoa dhabihu sadaka za amani
kwa BWANA: ng'ombe 22,000, pamoja na
kondoo na mbuzi 120,000. Hivyo ndivyo
mfalme na Waisraeli wote walivyoweka
wakfu Hekalu la BWANA.

64 Siku iyo hiyo mfalme akaweka wakfu
sehemu ya katikati ya ua uliokuwa mbele
ya Hekalu la BWANA na hapo akatoa
sadaka za kuteketezwa, sadaka za nafaka
na mafuta ya sadaka za amani, kwa sababu
madhabahu ya shaba iliyokuwa mbele za
BWANA ilikuwa ndogo sana kuweza kubeba
sadaka hizo za kuteketezwa, sadaka za
nafaka na mafuta ya sadaka ya amani.

65 Hivyo Solomoni akaiadhimisha sikukuu
kwa wakati ule, na Israeli wote pamoja
naye. Walikuwa kusanyiko kubwa sana,
watu kutoka Lebo-Hamathi hadi Kijito cha
Misri. Wakaiadhimisha mbele za BWANA
Mungu wetu kwa siku saba na siku saba
zaidi, yaani, jumla siku kumi na nne. 66 Siku
iliyofuata, aliwaruhusu watu waondoke.
Wakambariki mfalme, kisha wakaenda
nyumbani, wakiwa na mashangilio na
furaha rohoni kwa ajili ya mambo yote
mema ambayo BWANA ametenda kwa ajili
ya Daudi mtumishi wake na watu wake
Israeli.

*BWANA Anamtokea Solomoni*

**(2 Nyakati 7:11-22)**

9 [a]Solomoni alipomaliza kujenga Hekalu la
BWANA na jumba la kifalme, alipokwisha
kufanya yote aliyotaka kufanya, 2 [b]BWANA
akamtokea mara ya pili, kama alivyokuwa
amemtokea huko Gibeoni. 3 [c]BWANA
akamwambia:

"Nimesikia dua na maombi
uliyofanya mbele zangu, nimeliweka
wakfu Hekalu hili ambalo umelijenga,
kwa kuweka Jina langu humo milele.
Macho yangu na moyo wangu utakuwa
humo siku zote.

4 [de]"Kukuhusu wewe, kama
ukienenda kwa unyofu wa moyo
na uadilifu, kama baba yako
Daudi alivyofanya na kutenda yote
ninayoyaagiza kwa kutunza maagizo
yangu na sheria, 5 [f]nitakiimarisha kiti
chako cha enzi juu ya Israeli milele
kama nilivyomwahidi Daudi baba yako
niliposema, 'Hutakosa kamwe kuwa na
mtu kwenye kiti cha enzi cha Israeli.'

6 [g]"Lakini kama ninyi au wana
wenu mkigeukia mbali nami na
kuziacha amri na maagizo yangu

[a]**9:1** Neh 9:2; Mwa 19:38; Kum 20:17; Amu 3:5; Kum 12:30
[b]**9:2** Law 27:30; Ezr 10:2; 2Kor 6:14; Kut 22:31; Kum 7:3
[c]**9:3** Isa 15:2; Za 143:4
[d]**9:4** Za 119:120
[e]**9:4** Ezr 10:3; Kut 29:39
[f]**9:5** Kut 9:29; 29:41
[g]**9:6** Ufu 18:5; Dan 9:7; Isa 59:12

niliyowapa na kwenda kuitumikia
miungu mingine na kuiabudu, 7 [a]basi
nitakatilia mbali Israeli kutoka nchi
niliyowapa, nami nitalikataa Hekalu
hili nililolitakasa kwa ajili ya Jina
langu. Ndipo Israeli itakuwa kitu cha
kudharauliwa na watu na kuwa kitu
cha kudhihakiwa miongoni mwa watu
wote. 8 [b]Ingawa hekalu hili linavutia
sasa, wote watakaolipita watashangaa
na kudhihaki wakisema, ‘Kwa nini
BWANA amefanya kitu kama hiki katika
nchi hii na kwa Hekalu hili?’ 9 [c]Watu
watajibu, ‘Kwa sababu wamemwacha
BWANA Mungu wao, aliyewatoa baba
zao Misri, nao wamekumbatia miungu
mingine, wakaiabudu na kuitumikia,
ndiyo sababu BWANA ameyaleta maafa
haya yote juu yao.’ ”

*Shughuli Nyingine Za Solomoni*

**(2 Nyakati 8)**

10 [d]Miaka ishirini ilipopita, ambayo katika
hiyo Solomoni alijenga majengo haya
mawili, yaani Hekalu la BWANA na jumba
la kifalme, 11 [e]Mfalme Solomoni akampa
Hiramu mfalme wa Tiro miji ishirini katika
Galilaya, kwa sababu Hiramu alikuwa
amempatia mierezi yote, misunobari
na dhahabu yote aliyohitaji. 12 [f]Lakini
Hiramu alipotoka Tiro kwenda kuiona ile
miji ambayo Solomoni alikuwa amempa,
hakupendezwa nayo. 13 [g]Hiramu akauliza,
“Hii ni miji ya namna gani uliyonipa, ndugu
yangu?”

Naye akaiita nchi ya Kabul,[h] jina
lililoko hadi leo. 14 [i]Basi Hiramu alikuwa
amempelekea mfalme talanta 120[j] za
dhahabu.

15 [k]Haya ni maelezo kuhusu kazi za
kulazimishwa ambazo Mfalme Solomoni,
alivyowafanyiza watu ili kulijenga hekalu
la BWANA, na jumba lake la kifalme, na
Milo,[l] ukuta wa Yerusalemu, Hazori,
Megido na Gezeri. 16 (Farao mfalme wa
Misri alikuwa ameushambulia na kuuteka
mji wa Gezeri. Alikuwa ameuchoma moto.
Akawaua Wakanaani waliokuwa wakikaa
humo na kisha kuutoa kwa binti yake,
yaani mkewe Solomoni, kama zawadi ya
arusi. 17 Solomoni akaujenga tena Gezeri.)
Akajenga Beth-Horoni ya Chini, 18 akajenga
Baalathi na Tamari kwenye jangwa katika
eneo la nchi yake, 19 vilevile miji ya ghala
na miji kwa ajili ya magari yake na kwa ajili
ya farasi wake: chochote alichotaka kujenga
katika Yerusalemu, katika Lebanoni, na
katika eneo yote aliyotawala.

20 Watu wote waliosalia kutoka kwa
Waamori, Wahiti, Waperizi, Wahivi
na Wayebusi (mataifa haya hayakuwa
Waisraeli), 21 yaani, wazao wao waliobakia
katika nchi, ambao Waisraeli hawangeweza
kuwaangamiza kabisa: hawa Solomoni
akawalazimisha kuwa watumwa katika
shokoa, kama ilivyo hadi leo. 22 Lakini
Solomoni hakumfanya yeyote wa Waisraeli
kuwa mtumwa; wao ndio waliokuwa
wapiganaji wake, maafisa wake wa serikali,
maafisa wake, wakuu wake, majemadari wa
jeshi wa magari yake ya vita na wapanda
farasi. 23 Pia walikuwa maafisa wakuu
wasimamizi wa miradi ya Solomoni: maafisa
550 waliwasimamia watu waliofanya kazi.

24 Baada ya binti Farao kuja kutoka Mji
wa Daudi na kuingia jumba la kifalme
ambalo Solomoni alikuwa amemjengea,
akajenga Milo.

25 Solomoni akatoa dhabihu za
kuteketezwa na sadaka za amani mara tatu
kwa mwaka, juu ya madhabahu aliyokuwa

---

[a]**9:7** 2Nya 29:6; Eze 21:1-32; Kum 28:36-64; Za 106:6; 2Nya 19:2; Mwa 18:19
[b]**9:8** Isa 33:2; Za 13:3; Mhu 12:11; Mwa 45:7; Isa 22:23; Za 19:8
[c]**9:9** Neh 9:36; Kut 1:14; 2Fal 25:28; Zek 1:16-17; Ezr 7:28
[d]**9:10** Kum 11:8; Isa 1:19-20
[e]**9:11** Law 18:25-28; Kum 18:9; 1Fal 14:24
[f]**9:12** Kut 34:15; Kum 7:3; Mit 13:22; Kut 23:32-33; Amu 2:2; 2Pet 2:20; 2Kor 6:14
[g]**9:13** Ay 15:5; Za 103:10
[h]13 Kabul maana yake isiyofaa kitu.
[i]**9:14** Kum 9:8-14; Neh 13:27; Yn 5:14
[j]14 Talanta 120 za dhahabu ni sawa na tani 4.5.
[k]**9:15** Neh 9:33; Za 51:4; Rum 3:19; Isa 24:16; 1Fal 8:47; Dan 9:14; Za 130:3
[l]15 Milo maana yake Boma la Ngome, pia 9:24.

amejengea kwa ajili ya BWANA, akifukiza
uvumba mbele za BWANA pamoja na
dhabihu hizo, hivyo kutimiza kanuni za
hekalu.
26 Mfalme Solomoni pia akatengeneza
pia meli huko Esion-Geberi, ambayo iko
karibu na Elathi katika Edomu, kwenye
ukingo wa Bahari ya Shamu.[a] 27 Naye
Hiramu akawatuma watu wake; mabaharia
walioijua bahari, kuhudumu katika hizo
meli pamoja na watu wa Solomoni.
28 Wakasafiri kwa bahari mpaka Ofiri na
kurudi na talanta 420[b] za dhahabu, ambazo
walimkabidhi Mfalme Solomoni.

### *Malkia Wa Sheba Amtembelea Solomoni*

**(2 Nyakati 9:1-12)**

10 [c]Malkia wa Sheba aliposikia habari za
umaarufu wa Solomoni na uhusiano
wake na jina la BWANA, akaja kumjaribu
kwa maswali magumu. 2 [d]Alifika Yerusalemu
akiwa na msafara mkubwa sana: pamoja na
ngamia waliobeba vikolezi, kiasi kikubwa
cha dhahabu na vito vya thamani; alikuja
kwa Solomoni na kuzungumza naye kuhusu
yote ambayo alikuwa nayo moyoni mwake.
3 [e]Solomoni akamjibu maswali yake yote,
hakukuwa na jambo lolote lililokuwa gumu
kwa mfalme asiweze kumwelezea. 4 [f]Malkia
wa Sheba alipoona hekima yote ya Solomoni
na jumba la kifalme alilokuwa amejenga,
5 [g]chakula kilichokuwa mezani pake, jinsi
maafisa wake walivyokaa, wahudumu
katika majoho yao, wanyweshaji wake
na sadaka za kuteketezwa alizotoa katika
hekalu la BWANA, alipatwa na mshangao.
6 [h]Akamwambia mfalme, "Taarifa
niliyosikia kwenye nchi yangu mwenyewe
kuhusu mafanikio na hekima yako ni kweli.
7 Lakini sikuamini mambo haya hadi
nilipokuja na kuona kwa macho yangu
mwenyewe. Naam, sikuambiwa hata nusu
yake; katika hekima na mali umezidi sana
ile taarifa niliyoisikia. 8 [i]Heri watu wako!
Heri hawa maafisa wako wasimamao
mbele yako daima na kusikia hekima yako!
9 [j]Ahimidiwe BWANA Mungu wako, ambaye
amependezwa sana nawe na kukuweka juu
ya kiti cha ufalme cha Israeli. Kwa sababu
ya upendo wake BWANA wa milele ajili ya
Israeli, amekufanya mfalme, ili kudumisha
haki na uadilifu."
10 Naye akampa mfalme talanta 120[k] za
dhahabu, kiasi kikubwa sana cha vikolezi
na vito vya thamani. Haikuwahi kamwe
kuletwa tena vikolezi vingi hivyo kuletwa
kama vile malkia wa Sheba alivyompa
Mfalme Solomoni.
11 [l](Meli za Hiramu zilileta dhahabu
kutoka Ofiri; tena kutoka huko zilileta
shehena kubwa ya miti ya msandali na
vito vya thamani. 12 [m]Mfalme akatumia
miti ya msandali kuwa nguzo ya Hekalu
la BWANA na kwa jumba la kifalme, pia
kwa kutengeneza vinubi na zeze kwa ajili
ya waimbaji. Kiasi hicho kingi cha msandali
hakijawahi kuingizwa au kuonekana humo
tangu siku ile.)
13 Mfalme Solomoni akampa malkia wa
Sheba kila kitu alichotamani na kukiomba,
kando na vile mfalme alivyokuwa amempa
kwa ukarimu wake wa kifalme. Kisha
malkia akaondoka na kurudi katika nchi
yake, yeye na watumishi wake.

### *Fahari Ya Solomoni*

**(2 Nyakati 9:13-28)**

14 [n]Uzito wa dhahabu ambayo Solomoni

---

[a]26 Yaani Bahari Nyekundu au Bahari ya Mafunjo.
[b]28 Talanta 420 za dhahabu ni sawa na tani 14.
[c]**10:1** 2Nya 20:9; Dan 9:20
[d]**10:2** Ezr 9:2; Kut 34:13; Neh 13:27; Kum 30:8-10
[e]**10:3** 2Fal 11:17; 2Nya 34:31; Kut 34:16; Kum 7:2-3; Ezr 9:4; Za 119:53, 120; Isa 66:2
[f]**10:4** 1Nya 28:10; Isa 35:3-4
[g]**10:5** Neh 5:12; 13:25
[h]**10:6** Kum 9:18; Yn 3:7; Za 102:4
[i]**10:8** Law 27:28; Yos 6:19
[j]**10:9** 1Sam 12:18; Ezr 1:5
[k]10 Talanta 120 za dhahabu ni sawa na tani 4.5.
[l]**10:11** Kum 24:1; Mit 28:13; Mal 2:10-16; Yer 3:13; Isa 1:16-17; Rum 12:2
[m]**10:12** Yos 6:5
[n]**10:14** Kum 16:18; Hes 25:4; 2Nya 30:8; 2Fal 23:26; 2Nya 28:11-13; 29:10; 30:8; Za 78:38; Isa 12:1

alipokea kwa mwaka ulikuwa talanta 666,[a] 15 [b]mbali na mapato kutoka kwa wafanyabiashara na wachuuzi, na kutoka kwa wafalme wote wa Kiarabu na watawala wa nchi.

16 Mfalme Solomoni akatengeneza ngao kubwa 200 kwa dhahabu iliyofuliwa; kila ngao ilikuwa na dhahabu yenye uzito wa shekeli 600[c] 17 Akatengeneza pia ngao ndogo 300 za dhahabu iliyofuliwa, kila ngao ikiwa na uzito wa mane tatu[d] za dhahabu. Mfalme akaziweka katika Jumba la Kifalme la Msitu wa Lebanoni.

18 [e]Kisha mfalme akatengeneza kiti kikubwa cha kifalme kwa kutumia pembe za ndovu na kukifunika kwa dhahabu safi. 19 [f]Kiti hicho kilikuwa na ngazi sita na egemeo la nyuma lilikuwa la mviringo kwa juu. Pande zote za kiti kulikuwa na mahali pa kuegemeza mikono, na simba wawili wakisimama kando ya hiyo mikono. 20 [g]Simba kumi na wawili walisimama kwenye ngazi sita, mmoja katika kila upande wa kila ngazi. Hakuna kitu kama hicho kilichokuwa kimefanyika kwenye ufalme mwingine wowote. 21 [h]Vikombe vyote vya Mfalme Solomoni vya kunywea vilikuwa vya dhahabu na vyombo vyote vya nyumbani katika Jumba la Kifalme la Msitu wa Lebanoni vilikuwa vya dhahabu safi. Hakukuwa na kitu kilichotengenezwa kwa fedha, kwa sababu fedha ilionekana ya thamani ndogo siku za Solomoni. 22 [i]Mfalme alikuwa na meli nyingi za biashara[j] baharini zilizokuwa zikiandamana na meli za Hiramu. Kwa mara moja kila miaka mitatu zilirudi, zikiwa zimebeba dhahabu, fedha, pembe za ndovu na nyani wakubwa na wadogo.

23 [k]Mfalme Solomoni alikuwa mkuu zaidi kwa utajiri na hekima kuliko wafalme wote wa dunia. 24 [l]Dunia yote ikatafuta kukutana na Solomoni ili kusikia hekima ambayo Mungu alikuwa ameiweka katika moyo wake. 25 [m]Mwaka baada ya mwaka, kila mmoja ambaye alikuja alileta zawadi: vyombo vya fedha na dhahabu, majoho, silaha na vikolezi, farasi na nyumbu.

26 [n]Solomoni akakusanya magari ya vita na farasi. Alikuwa na magari 1,400 na farasi 12,000, ambayo aliyaweka katika miji ya magari na mengine akawa nayo huko Yerusalemu. 27 [o]Mfalme akafanya fedha kuwa kitu cha kawaida kama mawe huko Yerusalemu, mierezi akaifanya kuwa mingi kama mikuyu vilimani. 28 Farasi wa Solomoni waliletwa kutoka Misri na kutoka Kue.[p] Wafanyabiashara wa mfalme waliwanunua kutoka Kue. 29 [q]Waliagiza magari kutoka Misri kwa bei ya shekeli 600 za fedha[r] na farasi kwa shekeli 150.[s] Pia waliwauza nje kwa wafalme wote wa Wahiti na wa Waaramu.[t]

### *Wakeze Solomoni*

11 [u]Hata hivyo, Mfalme Solomoni akawapenda wanawake wengi wa kigeni zaidi, mbali na binti Farao: wanawake wa Wamoabu, Waamoni, Waedomu, Wasidoni na Wahiti. 2 [v]Walitoka katika mataifa ambayo BWANA aliwaambia Waisraeli, "Msije mkaoana nao, kwa kuwa hakika wataigeuza mioyo yenu mgeukie miungu yao." Hata hivyo, Solomoni akakaza kuwapenda. 3 [w]Alikuwa na wake 700

---

[a]14 Talanta 666 za dhahabu ni sawa na tani 25.
[b]**10:15** Neh 11:16
[c]16 Shekeli 600 za dhahabu ni sawa na kilo 3.5.
[d]17 Mane tatu za dhahabu ni sawa na kilo 1.7.
[e]**10:18** Ezr 5:2; 2:2; Amu 3:6; Zek 6:1
[f]**10:19** 2Fal 10:15; Law 5:15; 6:4-6; 1Nya 29:24; 2Nya 30:8; Gal 2:9; Mit 22:26
[g]**10:20** 1Nya 24:14
[h]**10:21** 1Nya 24:8
[i]**10:22** 1Nya 9:12
[j]22 Au: za Tarshishi (ona pia 1Fal 22:48; 2Nya 9:21; 20:36; Isa 2:16; 60:9).
[k]**10:23** Neh 8:7; 9:4
[l]**10:24** Neh 3:1; 12:10
[m]**10:25** Ezr 3:2; 8:3; Neh 7:13
[n]**10:26** Kum 17:16
[o]**10:27** Ay 27:16; 1Nya 27:28
[p]28 Yaani Kilikia ilioko Syria.
[q]**10:29** Hes 13:29
[r]29 Shekeli 600 za fedha ni sawa na kilo 7.
[s]29 Shekeli 150 za fedha ni sawa na kilo 1.7.
[t]29 Waaramu hapa ina maana ya Washamu.
[u]**11:1** Kut 34:16; 1Fal 12:21, 31
[v]**11:2** Kut 34:16; 1Fal 16:31
[w]**11:3** Mwa 22:24; Mit 31:3

mabinti wa uzao wa kifalme, na masuria
300, nao wake zake wakampotosha.
4 [a]Kadiri Solomoni alivyozidi kuzeeka,
wake zake wakaugeuza moyo wake
kuelekea miungu mingine, na moyo wake
haukujitolea kikamilifu kwa BWANA Mungu
wake, kama ulivyokuwa moyo wa Daudi
baba yake. 5 [b]Solomoni akafuata Ashtorethi
mungu mke wa Wasidoni, na Moleki[c] mungu
aliyekuwa chukizo la Waamoni. 6 [d]Kwa
hiyo Solomoni akafanya uovu machoni pa
BWANA; hakumfuata BWANA kikamilifu
kama alivyofanya Daudi baba yake.

7 [e]Kwenye kilima mashariki mwa
Yerusalemu, Solomoni akajenga mahali
pa juu kwa ajili ya Kemoshi chukizo la
Wamoabu, na kwa Moleki mungu chukizo
la Waamoni. 8 Akafanya hivyo kwa wake
zake wote wa kigeni, ambao walifukiza
uvumba na kutoa dhabihu kwa miungu yao.

9 [f]BWANA akamkasirikia Solomoni
kwa sababu moyo wake uligeuka mbali
na BWANA, Mungu wa Israeli, ambaye
alikuwa amemtokea mara mbili. 10 [g]Ingawa
alikuwa amemkataza Solomoni kufuata
miungu mingine, Solomoni hakutii amri ya
BWANA. 11 Kwa hiyo BWANA akamwambia
Solomoni, “Kwa kuwa hii ndiyo hali yako
na hukushika Agano langu na sheria zangu
nilizokuamuru, hakika nitaurarua ufalme
kutoka kwako na kumpa mmoja wa walio
chini yako. 12 Hata hivyo, kwa ajili ya Daudi
baba yako, sitafanya jambo hili wakati wa
uhai wako. Nitaurarua kutoka mikononi
mwa mwanao. 13 [h]Lakini pia sitaurarua
ufalme wote kutoka kwake, bali nitampa
kabila moja kwa ajili ya Daudi mtumishi
wangu na kwa ajili ya Yerusalemu, ambao
nimeuchagua.”

*Adui Za Solomoni*

14 Kisha BWANA akamwinua adui dhidi
ya Solomoni, Hadadi, Mwedomu, kutoka
ukoo wa ufalme wa Edomu. 15 [i]Huko nyuma
wakati Daudi alipokuwa akipigana na
Edomu, Yoabu jemadari wa jeshi, aliyekuwa
amekwenda kuzika waliouawa, alikuwa
amewaua wanaume wote waliokuwako
Edomu. 16 Yoabu na Waisraeli wote walikaa
huko kwa miezi sita, mpaka walipomaliza
kuwaangamiza wanaume wote huko
Edomu. 17 Lakini Hadadi, akiwa bado
mvulana mdogo, alikimbilia Misri akiwa na
baadhi ya maafisa wa Kiedomu waliokuwa
wakimhudumia baba yake. 18 [j]Wakaondoka
Midiani wakaenda Parani. Basi wakichukua
pamoja nao wanaume kutoka Parani,
wakaenda Misri, kwa Farao mfalme wa
Misri, ambaye alimpa Hadadi nyumba,
ardhi na akampatia chakula.

19 Farao akapendezwa sana na Hadadi
hata akampa ndugu wa mkewe mwenyewe,
Malkia Tapenesi, ili aolewe na Hadadi.
20 Huyo ndugu wa Tapenesi akamzalia
mwana aliyeitwa Genubathi, ambaye
alilelewa na Tapenesi katika jumba la
kifalme. Huko Genubathi aliishi pamoja
na watoto wa Farao mwenyewe.

21 Alipokuwa huko Misri, Hadadi alisikia
kwamba Daudi amepumzika na baba
zake na ya kwamba pia Yoabu aliyekuwa
jemadari wa jeshi amekufa. Ndipo Hadadi
akamwambia Farao, “Niruhusu niende ili
niweze kurudi katika nchi yangu.”

22 Farao akauliza, “Umekosa nini hapa,
kwamba unataka kurudi katika nchi yako?”

Hadadi akajibu, “Hakuna, lakini niruhusu
niende!”

23 [k]Mungu akamwinua adui mwingine
dhidi ya Solomoni, Rezoni mwana wa
Eliada, ambaye alikuwa amemkimbia
bwana wake Hadadezeri, mfalme wa
Soba. 24 [l]Akawakusanya watu, naye akawa
kiongozi wa kundi la waasi, wakati Daudi
alipoangamiza majeshi ya Soba; waasi
walikwenda Dameski, mahali walipokaa

[a]**11:4** Kut 34:16; 1Nya 29:19
[b]**11:5** Amu 2:13
[c]5 Moleki au Milkomu ni mungu aliyekuwa akiabudiwa na Waamoni; alikuwa chukizo kwa sababu watoto walitolewa kafara kwake.
[d]**11:6** Kum 4:25
[e]**11:7** 2Fal 23:13; Hes 21:29; Mdo 7:43
[f]**11:9** 1Fal 3:5
[g]**11:10** 1Fal 9:6; 6:12
[h]**11:13** 2Sam 7:15; Kum 12:11
[i]**11:15** 1Nya 18:12
[j]**11:18** Hes 10:12
[k]**11:23** 1Fal 5:4; 2Sam 8:3
[l]**11:24** 2Sam 8:5

na kumiliki. 25 [a]Rezoni alikuwa adui wa
Israeli kwa muda wote alioishi Solomoni,
ukiongezea matatizo yaliyosababishwa na
Hadadi. Kwa hiyo Rezoni akatawala katika
Aramu[b] na alikuwa mkatili kwa Israeli.

*Yeroboamu Anaasi Dhidi Ya Solomoni*

26 [c]Pia, Yeroboamu mwana wa Nebati
aliasi dhidi ya mfalme. Alikuwa mmoja wa
maafisa wa Solomoni, Mwefraimu kutoka
Sereda, ambaye mama yake alikuwa mjane
aliyeitwa Serua.
27 [d]Haya ndiyo maelezo ya jinsi
alivyomwasi mfalme: Solomoni alikuwa
amejenga Milo[e] naye akawa ameziba
mwanya katika ukuta wa mji wa Daudi
baba yake. 28 [f]Basi Yeroboamu alikuwa
mtu shujaa na hodari, naye Solomoni
alipoona jinsi kijana alivyofanya kazi yake,
akamweka kuwa kiongozi wa kazi yote ya
mikono ya nyumba ya Yosefu.
29 [g]Karibu na wakati ule Yeroboamu
alikuwa anatoka nje ya Yerusalemu, Ahiya
nabii Mshiloni akakutana naye njiani,
akiwa amevaa joho jipya. Hawa wawili
walikuwa peke yao mashambani, 30 [h]naye
Ahiya akachukua joho jipya alilokuwa
amevaa akalirarua vipande kumi na
viwili. 31 [i]Kisha akamwambia Yeroboamu,
“Chukua vipande kumi kwa ajili yako, kwa
kuwa hivi ndivyo BWANA, Mungu wa Israeli
asemavyo: ‘Tazama, ninakwenda kuuchana
ufalme kutoka mikononi mwa Solomoni na
kukupa wewe makabila kumi. 32 [j]Lakini kwa
ajili ya mtumishi wangu Daudi na mji wa
Yerusalemu, ambao nimeuchagua miongoni
mwa makabila yote ya Israeli, atakuwa na
kabila moja. 33 [k]Nitafanya hivi kwa sababu
wameniacha mimi na kuabudu Ashtorethi
mungu mke wa Wasidoni, Kemoshi mungu
wa Wamoabu, na Moleki mungu wa
Waamoni, nao hawakwenda katika njia
zangu ili kufanya yaliyo sawa machoni
pangu, wala kushika amri na sheria zangu
kama Daudi, babaye Solomoni, alivyofanya.
34 “ ‘Lakini sitauondoa ufalme wote
kutoka mikononi mwa Solomoni,
nimemfanya mtawala siku zote za maisha
yake kwa ajili ya Daudi mtumishi wangu,
niliyemchagua na ambaye aliyatunza
maagizo na amri zangu. 35 Nitauondoa
ufalme kutoka mikononi mwa mwanawe na
kukupa wewe makabila kumi. 36 [l]Nitampa
mwanawe kabila moja ili kwamba Daudi
mtumishi wangu awe na taa mbele zangu
daima katika Yerusalemu, mji ambao
nimeuchagua kuweka Jina langu. 37 [m]Hata
hivyo, kukuhusu wewe Yeroboamu,
nitakutwaa, nawe utatawala juu ya yote
yale moyo wako unayotamani, utakuwa
mfalme juu ya Israeli. 38 [n]Ikiwa utafanya
kila nitakalokuamuru, kuenenda katika njia
zangu na kufanya yaliyo sawa mbele za
macho yangu kwa kuzishika amri zangu
na maagizo yangu kama alivyofanya Daudi
mtumishi wangu, nitakuwa pamoja nawe.
Nitakujengea ufalme utakaodumu kama ule
niliomjengea Daudi, nami nitakupa Israeli.
39 Nitawatesa wazao wa Daudi kwa ajili ya
hili, lakini siyo milele.’ ”
40 [o]Solomoni akajaribu kumuua
Yeroboamu, lakini Yeroboamu akakimbilia
Misri, kwa Mfalme Shishaki, naye akakaa
huko mpaka Solomoni alipofariki.

*Kifo Cha Solomoni*

**(2 Nyakati 9:29-31)**

41 Kwa habari za matukio mengine ya
utawala wa Solomoni, yote aliyoyafanya na
hekima aliyoionyesha, je hayakuandikwa
yote katika kitabu cha matendo cha
Solomoni? 42 Solomoni alitawala Israeli
yote miaka arobaini, akiwa Yerusalemu.
43 Kisha Solomoni akalala pamoja na baba
zake, naye akazikwa katika mji wa Daudi

[a]**11:25** Mwa 10:22; 2Sam 10:19
[b]25 Yaani Shamu (ambayo leo ni Syria).
[c]**11:26** 2Nya 13:6
[d]**11:27** 1Fal 9:24
[e]27 Milo maana yake Boma la Ngome.
[f]**11:28** Rut 2:1; Mit 22:29
[g]**11:29** 1Fal 12:15; 14:2
[h]**11:30** 1Sam 15:27
[i]**11:31** 1Fal 11:11; 1Sam 15:27
[j]**11:32** 2Sam 7:15
[k]**11:33** Amu 2:13; 1Fal 3:3
[l]**11:36** 1Fal 12:17
[m]**11:37** 1Fal 14:7; 2Sam 3:21
[n]**11:38** Kum 12:25; 2Sam 3:15; Kut 1:21
[o]**11:40** 1Fal 12:2; 2Nya 10:2; 12:2

baba yake. Naye Rehoboamu mwanawe
akawa mfalme baada yake.

*Israeli Yaasi Dhidi Ya Rehoboamu*

**(2 Nyakati 10:1-19)**

12 [a]Rehoboamu akaenda Shekemu,
kwa kuwa Waisraeli wote walikuwa
wamekwenda huko kumfanya yeye kuwa
mfalme. 2 [b]Yeroboamu mwana wa Nebati
aliposikia hili (alikuwa bado yuko Misri
alikokuwa amekimbilia awe mbali na
Mfalme Solomoni), akarudi kutoka Misri.
3 Kwa hiyo wakatuma watu kumwita
Yeroboamu, yeye na kusanyiko lote la
Israeli wakamwendea Rehoboamu na
kumwambia, 4 [c]“Baba yako aliweka nira
nzito juu yetu, lakini sasa tupunguzie kazi
za kikatili na nira nzito aliyoweka juu yetu,
nasi tutakutumikia.”
5 Rehoboamu akajibu, “Nendeni kwa
muda wa siku tatu na kisha mnirudie.” Basi
watu wakaenda zao.
6 [d]Kisha Mfalme Rehoboamu akataka
shauri kwa wazee ambao walimtumikia
Solomoni baba yake wakati wa uhai wake
akawauliza, “Mnanishauri nini katika
kuwajibu watu hawa?”
7 [e]Wakajibu, “Kama leo utakuwa
mtumishi wa watu hawa na kuwahudumia
na kuwapa jibu linaloridhisha, watakuwa
watumishi wako daima.”
8 [f]Lakini Rehoboamu akakataa shauri
alilopewa na wazee na akataka ushauri
kwa vijana wanaume rika lake waliokuwa
wakimtumikia. 9 Akawauliza, “Ninyi
ushauri wenu ni nini? Tutawajibuje watu
hawa wanaoniambia, ‘Ifanye nyepesi nira
baba yako aliyoweka juu yetu?’ ”
10 Wale vijana wa rika lake wakamjibu,
“Waambie watu hawa waliokuambia, ‘Baba
yako aliweka nira nzito juu yetu, lakini
ifanye nira yetu nyepesi,’ kuwa, ‘Kidole
changu kidogo ni kinene kuliko kiuno cha
baba yangu. 11 Baba yangu aliweka nira
nzito juu yenu, mimi nitaifanya hata iwe
nzito zaidi. Baba yangu aliwachapa kwa
mijeledi, mimi nitawachapa kwa nge.’ ”
12 Siku tatu baadaye, Yeroboamu na
watu wote wakamrudia Rehoboamu, kama
mfalme alivyokuwa amesema, “Rudini
kwangu baada ya siku tatu.” 13 Mfalme
akawajibu watu kwa ukatili. Akikataa
shauri alilopewa na wazee, 14 [g]akafuata
shauri la vijana wa rika lake na kusema,
“Baba yangu alifanya nira yenu kuwa
nzito, mimi nitaifanya kuwa nzito zaidi.
Baba yangu aliwachapa kwa mijeledi,
mimi nitawachapa kwa nge.” 15 [h]Kwa hiyo
mfalme hakuwasikiliza watu, kwa kuwa
jambo hili lilitoka kwa BWANA, ili kutimiza
neno ambalo BWANA alikuwa amenena kwa
Yeroboamu mwana wa Nebati kupitia Ahiya
Mshiloni.
16 [i]Israeli wote walipoona kuwa mfalme
amekataa kuwasikiliza, wakamjibu mfalme:

“Tuna fungu gani kwa Daudi?
  Sisi hatuna urithi kwa mwana wa
    Yese.
Nendeni kwenye mahema yenu, ee
    Israeli!
  Angalia nyumba yako mwenyewe,
    ee Daudi!”

Hivyo Waisraeli wakaenda kwenye mahema
yao. 17 [j]Lakini kwa habari ya Waisraeli
waliokuwa wakiishi katika miji ya Yuda,
Rehoboamu akaendelea kuwatawala bado.
18 [k]Mfalme Rehoboamu akamtuma
Adoramu, aliyekuwa msimamizi wa wale
waliofanya kazi ngumu kwa kulazimishwa,
lakini Israeli wote wakampiga kwa mawe
hadi akafa. Hata hivyo, Mfalme Rehoboamu,
akafanikiwa kuingia kwenye gari lake na
kutorokea Yerusalemu. 19 [l]Hivyo Israeli
wakaasi dhidi ya nyumba ya Daudi hadi leo.
20 [m]Waisraeli wote waliposikia kwamba
Yeroboamu amerudi, wakatuma watu na

[a]**12:1** Mwa 12:6; Yos 24:32
[b]**12:2** 1Fal 11:40
[c]**12:4** 1Sam 8:11-18
[d]**12:6** 1Fal 4:2
[e]**12:7** Mit 15:1
[f]**12:8** Law 19:32
[g]**12:14** Kut 1:14
[h]**12:15** Kum 2:30; 1Fal 11:29
[i]**12:16** Mwa 31:14; Isa 7:17
[j]**12:17** 1Fal 11:36
[k]**12:18** 2Sam 20:24; Yos 7:25
[l]**12:19** 2Fal 17:21
[m]**12:20** 1Fal 11:13

kumwita kwenye kusanyiko na kumfanya mfalme juu ya Israeli yote. Ni kabila la Yuda peke yake lililobaki kuwa tiifu kwa nyumba ya Daudi.

21 [a]Ikawa Rehoboamu alipofika Yerusalemu, akakusanya nyumba yote ya Yuda na kabila la Benyamini, wanaume wapiganaji 180,000, kufanya vita dhidi ya nyumba ya Israeli na kuurudisha tena ufalme kwa Rehoboamu mwana wa Solomoni.

22 [b]Lakini neno hili la Mungu likamjia Shemaya mtu wa Mungu: 23 "Mwambie Rehoboamu mwana wa Solomoni mfalme wa Yuda, na nyumba yote ya Yuda na Benyamini, na watu wengine wote, 24 'Hili ndilo asemalo BWANA: Msipande kupigana dhidi ya ndugu zenu, Waisraeli. Nendeni nyumbani, kila mmoja wenu, kwa kuwa hili nimelitenda mimi.' " Kwa hiyo wakalitii neno la BWANA na kurudi nyumbani, kama BWANA alivyokuwa ameagiza.

*Ndamа Wa Dhahabu Huko Betheli Na Dani*

25 [c]Kisha Yeroboamu akajenga Shekemu akaizungushia ngome katika nchi ya vilima ya Efraimu na akaishi huko. Akatoka huko, akaenda akajenga Penueli.[d]

26 Yeroboamu akawaza moyoni mwake, "Sasa inawezekana ufalme ukarudi katika nyumba ya Daudi. 27 [e]Kama watu hawa watapanda kwenda kutoa dhabihu katika Hekalu la BWANA huko Yerusalemu, mioyo yao itamrudia bwana wao, Rehoboamu mfalme wa Yuda. Wataniua mimi na kurudi kwa Mfalme Rehoboamu."

28 [f]Baada ya kutafuta shauri, mfalme akatengeneza ndama wawili wa dhahabu. Akawaambia watu, "Ni gharama kubwa kwenu kukwea kwenda Yerusalemu. Hii hapa miungu yenu, ee Israeli, iliyowapandisha kutoka Misri." 29 [g]Ndama mmoja akamweka Betheli na mwingine Dani. 30 [h]Nalo jambo hili likawa dhambi, watu wakawa wanaenda hadi Dani kumwabudu huyo aliyewekwa huko.

31 [i]Yeroboamu akajenga madhabahu mahali pa juu pa kuabudia miungu na kuwateua makuhani kutoka watu wa aina zote, ijapokuwa hawakuwa Walawi. 32 [j]Pia Yeroboamu akaweka sikukuu katika siku ya kumi na tano ya mwezi wa nane, kama sikukuu iliyokuwa ikifanyika huko Yuda, na akatoa dhabihu juu ya madhabahu. Akafanya hivyo huko Betheli akitoa dhabihu kwa ndama alizotengeneza. Huko Betheli akawaweka makuhani, na pia katika sehemu za juu za kuabudia miungu alizozitengeneza. 33 [k]Katika siku ya kumi na tano ya mwezi wa nane, mwezi aliouchagua mwenyewe, alitoa dhabihu juu ya madhabahu aliyokuwa amejenga huko Betheli. Kwa hiyo akaweka sikukuu kwa ajili ya Waisraeli na akapanda madhabahuni kutoa sadaka.

*Mtu Wa Mungu Kutoka Yuda*

13 [l]Kwa neno la BWANA, mtu wa Mungu alifika Betheli kutoka Yuda wakati Yeroboamu alipokuwa amesimama kando ya madhabahu ili kutoa sadaka. 2 [m]Akapiga kelele dhidi ya madhabahu kwa neno la BWANA: "Ee madhabahu, madhabahu! Hivi ndivyo asemavyo BWANA: 'Mwana aitwaye Yosia atazaliwa katika nyumba ya Daudi. Juu yako atawatoa dhabihu makuhani wa mahali pa juu pa kuabudia miungu wale ambao wanatoa sadaka hapa sasa, nayo mifupa ya wanadamu itachomwa juu yako.' " 3 [n]Siku iyo hiyo, mtu wa Mungu akatoa ishara: "Hii ndiyo ishara BWANA aliyotangaza: Madhabahu haya yatapasuka na majivu yaliyo juu yake yatamwagika."

4 Mfalme Yeroboamu aliposikia kile mtu wa Mungu alichosema, alipopiga kelele dhidi ya madhabahu huko

[a]**12:21** 2Nya 11:1
[b]**12:22** 2Nya 12:5-7; Kum 33:1; 2Fal 4:7
[c]**12:25** Amu 8:8
[d]25 Jina lingine ni Penieli kwa Kiebrania.
[e]**12:27** Kum 12:5-6
[f]**12:28** Kut 32:4; 2Nya 11:15
[g]**12:29** Amu 18:27-31; Amo 8:14
[h]**12:30** 1Fal 13:34; 2Fal 17:21
[i]**12:31** Law 26:30; 2Fal 17:32; 2Nya 11:14-15
[j]**12:32** Hes 29:12; 2Fal 10:29
[k]**12:33** 2Fal 23:15; Amo 7:13
[l]**13:1** Kum 33:1; Amo 7:13
[m]**13:2** 2Fal 23:15-16, 20; Law 26:30
[n]**13:3** Mwa 24:14; Yn 2:11

Betheli, akanyoosha mkono wake kutoka
madhabahuni na kusema, "Mkamate!"
Lakini mkono aliokuwa ameunyoosha
kumwelekea yule mtu ukasinyaa na
kubaki hapo hapo, kiasi kwamba hakuweza
kuurudisha. 5 Pia, madhabahu yalipasuka
na majivu yakamwagika sawasawa na
ishara iliyotolewa na mtu wa Mungu kwa
neno la Bwana.

6 [a]Kisha mfalme akamwambia mtu wa
Mungu, "Niombee kwa Bwana Mungu
wako ili mkono wangu upate kupona." Kwa
hiyo mtu wa Mungu akamwombea kwa
Bwana, nao mkono wa mfalme ukapona
na kuwa kama ulivyokuwa hapo kwanza.

7 [b]Mfalme akamwambia yule mtu wa
Mungu, "Twende nyumbani kwangu upate
chakula, nami nitakupa zawadi."

8 [c]Lakini yule mtu wa Mungu akamjibu
mfalme, "Hata kama ungenipa nusu ya mali
zako, nisingekwenda pamoja na wewe, wala
nisingekula mkate au kunywa maji hapa.
9 Kwa kuwa niliagizwa kwa neno la Bwana:
'Kamwe usile mkate wala usinywe maji au
kurudi kwa njia uliyojia.' " 10 Kwa hiyo
akafuata njia nyingine na hakurudi kupitia
njia ile ambayo alikuwa ameijia Betheli.

11 Basi kulikuwepo na nabii fulani
mzee aliyekuwa anaishi Betheli, ambaye
wanawe walikuja kumwambia yote ambayo
mtu wa Mungu alikuwa ameyafanya pale
siku ile. Pia wakamwambia baba yao
yale aliyomwambia mfalme. 12 Baba yao
akawauliza, "Ameelekea njia gani?" Nao
wanawe wakamwonyesha ile njia yule mtu
wa Mungu kutoka Yuda aliyopita. 13 Hivyo
akawaambia wanawe, "Nitandikieni
punda." Walipokwisha kumtandikia punda,
akampanda 14 na kumfuatilia yule mtu
wa Mungu. Akamkuta ameketi chini ya
mwaloni na akamuuliza, "Je, wewe ndiwe
mtu wa Mungu kutoka Yuda?"

Akamjibu, "Mimi ndiye."

15 Basi nabii akamwambia, "Karibu
nyumbani pamoja na mimi ule."

16 [d]Yule mtu wa Mungu akasema, "Siwezi
kurudi na kwenda nawe, wala siwezi kula
mkate au kunywa maji pamoja nawe mahali
hapa. 17 Nimeambiwa kwa neno la Bwana:
'Kamwe usile mkate au kunywa maji huko
au kurudia njia uliyojia.' "

18 [e]Yule nabii mzee akajibu, "Mimi pia ni
nabii, kama wewe. Naye malaika alisema
nami kwa neno la Bwana: 'Mrudishe
aje katika nyumba yako ili apate kula
mkate na kunywa maji.' " (Lakini alikuwa
akimwambia uongo.) 19 Hivyo mtu wa
Mungu akarudi pamoja naye na akala na
kunywa katika nyumba yake.

20 Wakati walipokuwa wameketi mezani,
neno la Bwana likamjia yule nabii mzee
aliyemrudisha huyo mtu wa Mungu.
21 [f]Akampazia sauti yule mtu wa Mungu
aliyekuwa ametoka Yuda, "Hivi ndivyo
asemavyo Bwana: 'Umeasi neno la Bwana
na hukushika amri uliyopewa na Bwana
Mungu wako, 22 bali ulirudi na ukala mkate
na kunywa maji mahali ambapo alikuambia
usile wala usinywe. Kwa hiyo maiti yako
haitazikwa katika kaburi la baba zako.' "

23 Wakati huyo mtu wa Mungu alipomaliza
kula na kunywa, nabii aliyekuwa
amemrudisha akamtandikia punda
wake. 24 [g]Alipokuwa akienda akakutana
na simba njiani, akamuua na maiti yake
ikabwagwa barabarani, yule punda wake na
simba wakiwa wamesimama karibu yake.
25 Baadhi ya watu waliopita pale waliona
maiti imebwagwa pale chini, simba akiwa
amesimama kando ya maiti, wakaenda na
kutoa habari katika mji ambao nabii mzee
aliishi.

26 [h]Yule nabii aliyekuwa amemrudisha
kutoka safari yake aliposikia habari hii
akasema, "Ni yule mtu wa Mungu ambaye
aliasi neno la Bwana. Bwana amemtoa
kwa simba, ambaye amemrarua na kumuua,
sawasawa na neno la Bwana lilivyokuwa
limemwonya."

27 Nabii akawaambia wanawe,
"Nitandikieni punda," nao wakafanya
hivyo. 28 Kisha akatoka akaenda akakuta

[a]**13:6** Mwa 20:7; Mdo 8:24
[b]**13:7** 1Sam 9:7
[c]**13:8** Hes 22:18
[d]**13:16** 1Fal 13:8
[e]**13:18** 1Fal 22:6; Mwa 19:14
[f]**13:21** 1Sam 13:14
[g]**13:24** 1Fal 20:36
[h]**13:26** 1Fal 13:21

maiti imebwagwa chini barabarani, punda
na simba wakiwa wamesimama kando
yake. Simba hakuwa amekula ile maiti
wala kumrarua punda. 29 Basi yule nabii
mzee akachukua maiti ya mtu wa Mungu,
akailaza juu ya punda na akairudisha katika
mji wake, ili amwombolezee na kumzika.
30 [a]Kisha akailaza ile maiti katika kaburi
lake huyo nabii mzee, nao wakaomboleza
juu yake na kusema, "Ee ndugu yangu!"
31 [b]Baada ya kumzika, akawaambia
wanawe, "Wakati nitakapokufa, mnizike
kwenye kaburi alimozikwa huyu mtu
wa Mungu; lazeni mifupa yangu kando
ya mifupa yake. 32 [c]Kwa maana ujumbe
alioutangaza kwa neno la Bwana dhidi
ya madhabahu huko Betheli na dhidi ya
madhabahu yote katika mahali pa juu pa
kuabudia miungu katika miji ya Samaria,
hakika yatatokea kweli."
33 Hata baada ya haya, Yeroboamu
hakubadili njia zake mbaya, lakini mara
nyingine tena akaweka makuhani kwa
ajili ya mahali pa juu pa kuabudia miungu
kutoka watu wa aina zote. Yeyote aliyetaka
kuwa kuhani alimweka wakfu kwa ajili
ya mahali pa juu pa kuabudia miungu.
34 [d]Hii ilikuwa ndiyo dhambi ya nyumba
ya Yeroboamu ambayo iliisababishia
kuanguka na kuangamia kwake hadi
kutoweka kwenye uso wa dunia.

### *Unabii Wa Ahiya Dhidi Ya Yeroboamu*

14 Wakati ule Abiya mwana wa
Yeroboamu akaugua, 2 [e]naye
Yeroboamu akamwambia mke wake,
"Nenda ukajibadilishe, ili watu wasijue
kwamba wewe ni mke wa Yeroboamu.
Kisha uende Shilo. Nabii Ahiya yuko huko,
yule aliyeniambia kuwa nitakuwa mfalme
juu ya watu hawa. 3 [f]Chukua mikate kumi,
maandazi kadhaa na gudulia la asali na
umwendee. Atakuambia kitakachotokea
kwa kijana." 4 Basi mke wa Yeroboamu
akafanya kama alivyosema mumewe,
akaenda kwenye nyumba ya Ahiya huko
Shilo.
Wakati huu Ahiya alikuwa kipofu
naye alishindwa kuona kwa sababu ya
umri wake. 5 Lakini Bwana alikuwa
amemwambia Ahiya, "Mke wa Yeroboamu
anakuja kukuuliza kuhusu mwanawe, kwa
kuwa ni mgonjwa, nawe utamjibu hivi na
hivi. Atakapowasili, atajifanya kuwa ni mtu
mwingine."
6 Hivyo Ahiya aliposikia kishindo cha
hatua zake mlangoni, akasema, "Karibu
ndani, mke wa Yeroboamu. Kwa nini
kujibadilisha? Nimetumwa kwako nikiwa
na habari mbaya. 7 [g]Nenda, ukamwambie
Yeroboamu kwamba hivi ndivyo asemavyo
Bwana, Mungu wa Israeli: 'Nilikuinua
miongoni mwa watu na kukufanya kiongozi
juu ya watu wangu Israeli. 8 [h]Nikararua
ufalme kutoka kwa nyumba ya Daudi
na kukupa wewe, lakini hukuwa kama
mtumishi wangu Daudi, ambaye aliyashika
maagizo yangu na kunifuata kwa moyo
wake wote, akifanya tu lile lililokuwa
sawa machoni pangu. 9 [i]Umefanya maovu
mengi kuliko wote waliokutangulia.
Umejitengenezea miungu mingine, sanamu
za chuma, umenighadhibisha na kunitupa
nyuma yako.
10 [j]" 'Kwa sababu ya hili, nitaleta maafa
juu ya nyumba ya Yeroboamu. Nitakatilia
mbali kutoka kwa Yeroboamu kila mzaliwa
wa mwisho wa kiume katika Israeli,
mtumwa au mtu huru. Nitachoma nyumba
ya Yeroboamu mpaka iteketee yote kama
mtu achomaye kinyesi. 11 [k]Mbwa watawala
wale walio wa nyumba ya Yeroboamu
watakaofia ndani ya mji na ndege wa
angani watajilisha kwa wale watakaofia
mashambani. Bwana amesema!'
12 "Kukuhusu wewe, rudi nyumbani.
Wakati utakapotia mguu katika mji
wako, kijana atakufa. 13 [l]Israeli yote

---

[a]**13:30** Yer 22:18
[b]**13:31** 2Fal 23:18
[c]**13:32** Law 26:30; 1Fal 16:24, 28
[d]**13:34** 1Fal 14:10; Yer 35:17
[e]**14:2** 1Fal 11:29
[f]**14:3** 1Sam 9:7
[g]**14:7** 1Sam 15:29
[h]**14:8** 1Sam 15:27; 1Fal 3:3
[i]**14:9** 2Nya 11:15; Za 50:17
[j]**14:10** Kum 32:36; 1Fal 15:29
[k]**14:11** 1Fal 16:4; Mwa 40:19
[l]**14:13** 2Nya 12:12; 19:3

itamwombolezea na kumzika. Kwa sababu
ni yeye pekee wa nyumba ya Yeroboamu
atakayezikwa, kwa sababu ni yeye peke
yake ndani ya nyumba ya Yeroboamu
ambaye BWANA, Mungu wa Israeli, ameona
kitu chema kwake.

14 "BWANA atajiinulia mwenyewe mfalme
juu ya Israeli ambaye ataikatilia mbali
jamaa ya Yeroboamu. Siku ndiyo hii! Nini?
Naam, hata sasa hivi. 15 [a]Naye BWANA
ataipiga Israeli, hata iwe kama unyasi
unaosukwasukwa juu ya maji. Ataing'oa
Israeli kutoka nchi hii nzuri aliyowapa baba
zao na kuwatawanya ng'ambo ya Mto Frati,
kwa sababu wamemghadhibisha BWANA
kwa kutengeneza nguzo za Ashera[b] 16 [c]Naye
atawaacha Israeli kwa ajili ya makosa ya
Yeroboamu aliyoyatenda na kusababisha
Israeli kuyatenda."

17 [d]Kisha mke wa Yeroboamu akainuka,
akaondoka kwenda Tirsa. Mara
alipokanyaga kizingiti cha mlango,
kijana akafa. 18 Wakamzika na Israeli
yote ikamwombolezea, kama BWANA
alivyokuwa amesema kupitia mtumishi
wake, nabii Ahiya.

19 Matukio mengine ya utawala
wa Yeroboamu, vita vyake na jinsi
alivyotawala, vimeandikwa katika kitabu
cha kumbukumbu za wafalme wa Israeli.
20 Yeroboamu akawatawala kwa miaka
ishirini na miwili, kisha akalala na baba
zake. Naye Nadabu mwanawe akawa
mfalme baada yake.

*Rehoboamu Mfalme Wa Yuda*

**(2 Nyakati 11:5–12:15)**

21 Rehoboamu mwana wa Solomoni
alikuwa mfalme wa Yuda. Alikuwa na
umri wa miaka arobaini na moja alipoanza
kutawala, naye akatawala miaka kumi na
saba huko Yerusalemu, mji ambao BWANA
alikuwa ameuchagua kutoka makabila yote
ya Israeli ili apate kuliweka humo Jina lake.
Mama yake aliitwa Naama, ambaye alikuwa
Mwamoni.

22 [e]Yuda wakatenda maovu machoni
pa BWANA. Kwa dhambi walizotenda
wakachochea hasira yake yenye wivu
zaidi kuliko baba zao walivyofanya. 23 [f]Pia
wakajijengea mahali pa juu pa kuabudia
miungu, mawe ya kuabudiwa na nguzo za
Ashera juu ya kila kilima kilichoinuka na
kila mti uliotanda. 24 [g]Walikuwepo hata
wanaume mahanithi wa mahali pa ibada
za sanamu katika nchi; watu wakajiingiza
katika kutenda machukizo ya mataifa
ambayo BWANA aliyafukuza mbele ya
Waisraeli.

25 [h]Katika mwaka wa tano wa utawala
wa Mfalme Rehoboamu, Shishaki mfalme
wa Misri akashambulia Yerusalemu.
26 [i]Akachukua hazina za Hekalu la
BWANA na hazina za jumba la kifalme.
Akachukua kila kitu, pamoja na zile ngao
zote za dhahabu ambazo Solomoni alikuwa
amezitengeneza. 27 [j]Kwa hiyo Mfalme
Rehoboamu akatengeneza ngao za shaba
badala ya zile za dhahabu na kuzikabidhi
kwa majemadari wa ulinzi wa zamu kwenye
ingilio la jumba la mfalme. 28 Kila wakati
mfalme alipokwenda katika Hekalu la
BWANA, walinzi walizichukua hizo ngao,
na baadaye walizirudisha kwenye chumba
cha ulinzi.

29 Kwa matukio mengine ya utawala
wa Rehoboamu na yote aliyoyafanya,
je, hayakuandikwa katika kitabu cha
kumbukumbu za wafalme wa Yuda?
30 [k]Kulikuwa na vita vinavyoendelea kati
ya Rehoboamu na Yeroboamu. 31 [l]Naye
Rehoboamu akalala na baba zake, na
akazikwa pamoja nao katika Mji wa Daudi.
Mama yake aliitwa Naama, ambaye alikuwa
Mwamoni. Naye Abiya[m] mwanawe akawa
mfalme baada yake.

---

[a]**14:15** Yer 44:3; Kum 12:3
[b]15 Yaani mfano wa mungu wa kike Ashera.
[c]**14:16** 1Fal 12:30
[d]**14:17** 1Fal 15:33; Yos 12:24
[e]**14:22** 2Nya 12:1; Kum 32:21
[f]**14:23** Kut 23:24; Kum 12:3
[g]**14:24** Mit 21:27; Kum 23:17
[h]**14:25** 2Nya 12:2
[i]**14:26** 1Fal 15:15, 18; 2Sam 8:7
[j]**14:27** 2Fal 11:5
[k]**14:30** 1Fal 12:21
[l]**14:31** 1Fal 11:1
[m]31 Maandishi mengine ya Kiebrania yanamwita Abiyamu.

*Abiya Mfalme Wa Yuda*

**(2 Nyakati 13:1–14:1)**

15 Katika mwaka wa kumi na nane wa
utawala wa Yeroboamu mwana wa
Nebati, Abiya akawa mfalme wa Yuda,
2 [a]naye akatawala huko Yerusalemu miaka
mitatu. Mama yake aliitwa Maaka binti
Abishalomu.[b]

3 [c]Alitenda dhambi zote baba yake
alizotenda kabla yake; moyo wake haukuwa
mkamilifu kwa BWANA Mungu wake kama
moyo wa Daudi baba yake ulivyokuwa.
4 [d]Pamoja na hayo, kwa ajili ya Daudi,
BWANA Mungu wake akampa taa katika
Yerusalemu kwa kumwinua mwana atawale
badala yake na kwa kuifanya Yerusalemu
kuwa imara. 5 [e]Kwa kuwa Daudi alifanya
yaliyo mema machoni pa BWANA na
hakushindwa kushika maagizo yote ya
BWANA siku zote za uhai wake, isipokuwa
katika habari ya Uria, Mhiti.

6 [f]Kulikuwa na vita kati ya Rehoboamu
na Yeroboamu wakati wote wa maisha
ya Abiya. 7 Kwa habari ya matukio
mengine ya utawala wa Abiya na yote
aliyofanya, je, hayakuandikwa katika
kitabu cha kumbukumbu za wafalme wa
Yuda? Kulikuwa na vita kati ya Abiya na
Yeroboamu. 8 Naye Abiya akalala na baba
zake akazikwa katika Mji wa Daudi. Asa
mwanawe akawa mfalme baada yake.

*Asa Mfalme Wa Yuda*

**(2 Nyakati 15:16–16:6)**

9 Katika mwaka wa ishirini wa utawala wa
Yeroboamu mfalme wa Israeli, Asa akawa
mfalme wa Yuda, 10 naye akatawala katika
Yerusalemu miaka arobaini na mmoja. Bibi
yake aliitwa Maaka binti Abishalomu.

11 [g]Asa akatenda yaliyo mema machoni
mwa BWANA, kama alivyokuwa ametenda
Daudi baba yake. 12 [h]Akawafukuza mahanithi
wa mahali pa kuabudia miungu kutoka nchi
na kuondoa sanamu zote ambazo baba
zake walikuwa wametengeneza. 13 Hata
akamwondoa bibi yake Maaka kwenye
wadhifa wake kama mama malkia, kwa
sababu alikuwa ametengeneza nguzo ya
Ashera ya kuchukiza. Asa akaikata hiyo
nguzo na kuiteketeza kwa moto katika
Bonde la Kidroni. 14 [i]Ijapokuwa hakuondoa
mahali pa juu pa kuabudia miungu, moyo
wa Asa ulikuwa umejiweka kwa BWANA
kikamilifu maisha yake yote. 15 [j]Akaleta
ndani ya Hekalu la BWANA fedha na
dhahabu na vile vyombo ambavyo yeye na
baba yake walikuwa wameviweka wakfu.

16 [k]Kulikuwa na vita kati ya Asa na Baasha
mfalme wa Israeli siku zote za utawala wao.
17 [l]Mfalme Baasha wa Israeli akashambulia
Yuda na kuweka ngome mji wa Rama ili
kumzuia yeyote asitoke wala kuingia nchi
ya Mfalme Asa wa Yuda.

18 [m]Kisha Asa akachukua fedha yote
na dhahabu iliyokuwa imeachwa katika
hazina za Hekalu la BWANA na za jumba
lake mwenyewe la kifalme. Akawakabidhi
maafisa wake na kuwatuma kwa Ben-
Hadadi mwana wa Tabrimoni, mwana wa
Hezioni, mfalme wa Aramu,[n] aliyekuwa
akitawala Dameski. 19 "Akasema na pawepo
mkataba kati yangu na wewe, kama
ulivyokuwepo kati ya baba yangu na baba
yako. Tazama, nimekuletea zawadi ya fedha
na dhahabu. Sasa vunja mkataba wako na
Baasha mfalme wa Israeli ili aniondokee
mimi."

20 Ben-Hadadi akakubaliana na Mfalme
Asa na kutuma majemadari wa majeshi
yake dhidi ya miji ya Israeli. Akaishinda
miji ya Iyoni, Dani, Abel-Beth-Maaka na
Kinerethi yote, pamoja na Naftali. 21 Wakati
Baasha aliposikia hili, akaacha kuijenga

---

[a] **15:2** 2Nya 11:20
[b] 2 Yaani Absalomu, maana yake Baba wa amani.
[c] **15:3** 1Fal 8:61
[d] **15:4** 2Sam 21:17
[e] **15:5** 2Sam 11:2-27
[f] **15:6** 1Fal 12:21; 2Nya 16:9
[g] **15:11** 1Fal 9:4
[h] **15:12** 1Fal 14:24
[i] **15:14** 2Nya 14:5; 1Fal 8:61
[j] **15:15** 2Sam 8:11
[k] **15:16** 1Fal 12:21
[l] **15:17** Yos 18:25
[m] **15:18** Yoe 3:5; Yer 49:27
[n] 18 Yaani Shamu (ambayo leo ni Syria).

Rama na akaenda kuishi Tirsa. [22] [a]Kisha
Mfalme Asa akatoa amri kwa Yuda yote,
pasipo kumbagua hata mmoja, kubeba
mawe na mbao kutoka Rama, ambazo
Baasha alikuwa akitumia huko. Mfalme
Asa akazitumia kujengea Geba iliyoko
Benyamini na Mispa pia.

[23] Kwa matukio yote ya utawala wa Asa,
mafanikio yake yote, yote aliyofanya na
miji aliyoijenga, je, hayakuandikwa katika
kitabu cha kumbukumbu za wafalme wa
Yuda? Katika uzee wake, hata hivyo, alipata
ugonjwa wa miguu. [24] [b]Kisha Asa akalala
pamoja na baba zake na kuzikwa pamoja
nao katika mji wa Daudi baba yake. Naye
Yehoshafati mwanawe akawa mfalme
baada yake.

*Nadabu Mfalme Wa Israeli*

[25] Nadabu mwana wa Yeroboamu akawa
mfalme wa Israeli katika mwaka wa pili
wa utawala wa Mfalme Asa wa Yuda,
naye akatawala Israeli kwa miaka miwili.
[26] [c]Akafanya maovu machoni pa Bwana,
akienenda katika njia za baba yake na
katika dhambi yake, ambayo alisababisha
Israeli kuifanya.

[27] [d]Baasha mwana wa Ahiya wa nyumba
ya Isakari akafanya shauri baya dhidi
yake, naye akamuua huko Gibethoni, mji
wa Wafilisti, wakati Nadabu na Israeli
yote walipokuwa wameuzingira. [28] Baasha
akamuua Nadabu katika mwaka wa tatu
wa utawala wa Asa mfalme wa Yuda, naye
Baasha akaingia mahali pake kuwa mfalme.

[29] Mara tu alipoanza kutawala, aliua
jamaa yote ya Yeroboamu. Hakumwachia
Yeroboamu yeyote aliyekuwa hai, bali
aliwaangamiza wote, kulingana na neno la
Bwana lililotolewa kupitia kwa mtumishi
wake Ahiya Mshiloni, [30] kwa sababu ya
dhambi alizokuwa amezitenda Yeroboamu
na kusababisha Israeli kuzitenda, tena kwa
sababu alimkasirisha Bwana, Mungu wa
Israeli.

[31] Kwa matukio mengine ya utawala
wa Nadabu na yote aliyofanya, je
hayakuandikwa katika kitabu cha
kumbukumbu za wafalme wa Israeli?
[32] Kulikuwa na vita kati ya Asa na Baasha
mfalme wa Israeli wakati wote wa utawala
wao.

*Baasha Mfalme Wa Israeli*

[33] Katika mwaka wa tatu wa utawala
wa Asa mfalme wa Yuda, Baasha mwana
wa Ahiya akawa mfalme wa Israeli yote
huko Tirsa, naye akatawala kwa miaka
ishirini na minne. [34] Akatenda maovu
machoni pa Bwana, akienenda katika njia
za Yeroboamu na dhambi yake, ambayo
alikuwa amesababisha Israeli kuitenda.

16 [e]Ndipo neno la Bwana likamjia Yehu
mwana wa Hanani dhidi ya Baasha,
kusema: [2] [f]"Nilikuinua kutoka mavumbini
na kukufanya kiongozi wa watu wangu
Israeli, lakini ukaenenda katika njia za
Yeroboamu na kusababisha watu wangu
Israeli kutenda dhambi na kunikasirisha
kwa dhambi zao. [3] [g]Basi nitamwangamiza
Baasha pamoja na nyumba yake, nami
nitaifanya nyumba yako kama ile ya
Yeroboamu mwanawe Nebati. [4] [h]Mbwa
watawala watu wa Baasha watakaofia mjini
na ndege wa angani watajilisha kwa wale
watakaofia mashambani."

[5] Kwa matukio mengine ya utawala
wa Baasha, aliyoyafanya na mafanikio
yake, je, hayakuandikwa katika kitabu
cha kumbukumbu za wafalme wa Israeli?
[6] Baasha akalala na baba zake naye
akazikwa huko Tirsa. Naye Ela mwanawe
akawa mfalme baada yake.

[7] [i]Zaidi ya hayo, neno la Bwana likamjia
Baasha pamoja na nyumba yake kupitia
kwa nabii Yehu mwana wa Hanani, kwa
sababu ya maovu yote aliyokuwa ametenda
machoni pa Bwana, akamkasirisha
kwa mambo aliyotenda, na kuwa kama
nyumba ya Yeroboamu, na pia kwa sababu
aliiangamiza.

[a]**15:22** Yos 18:24; 2Fal 23:8
[b]**15:24** Mt 1:8
[c]**15:26** 1Fal 12:30; Kum 4:25
[d]**15:27** 1Fal 14:14; Yos 19:44
[e]**16:1** 1Fal 16:7; 2Nya 19:2
[f]**16:2** 1Fal 14:7-9
[g]**16:3** 1Fal 16:11; 21:22
[h]**16:4** 1Fal 14:11
[i]**16:7** 1Fal 16:11

*Ela Mfalme Wa Israeli*

8 Katika mwaka wa ishirini na sita wa
utawala wa Asa mfalme wa Yuda, Ela
mwana wa Baasha akawa mfalme wa
Israeli, naye akatawala huko Tirsa kwa
miaka miwili.
9 [a]Zimri, mmoja wa maafisa wake,
aliyekuwa na amri juu ya nusu ya magari
yake ya vita, akafanya hila mbaya dhidi ya
Ela. Wakati huo Ela alikuwa Tirsa, akilewa
katika nyumba ya Arsa, mtu aliyekuwa
msimamizi wa jumba la kifalme huko Tirsa.
10 [b]Zimri akaingia, akampiga na kumuua
katika mwaka wa ishirini na saba wa
utawala wa Asa mfalme wa Yuda. Kisha
Zimri akaingia mahali pake kuwa mfalme.
11 Mara tu alipoanza kutawala na kuketi
juu ya kiti cha ufalme, aliua jamaa yote
ya Baasha. Hakumwacha mwanaume hata
mmoja, akiwa ni ndugu au rafiki. 12 Hivyo
Zimri akaangamiza jamaa yote ya Baasha,
kulingana na neno la Bwana lililonenwa
dhidi ya Baasha kupitia nabii Yehu:
13 [c]kwa sababu ya dhambi zote Baasha na
mwanawe Ela walizokuwa wametenda
na wakasababisha Israeli kuzitenda, basi
wakamkasirisha Bwana, Mungu wa Israeli
kwa sanamu zao zisizofaa.
14 Kwa matukio mengine ya utawala wa
Ela, na yote aliyoyafanya, je, hayakuandikwa
katika kitabu cha kumbukumbu za wafalme
wa Israeli?

*Zimri Mfalme Wa Israeli*

15 [d]Katika mwaka wa ishirini na saba
wa utawala wa Asa mfalme wa Yuda,
Zimri akatawala huko Tirsa siku saba.
Jeshi lilikuwa limepiga kambi karibu na
Gibethoni, mji wa Wafilisti. 16 Wakati
Waisraeli waliokuwa kambini waliposikia
kuwa Zimri alikuwa amefanya hila mbaya
dhidi ya mfalme na kumuua, wakamtangaza
Omri, jemadari wa jeshi, kuwa mfalme
wa Israeli siku iyo hiyo huko kambini.
17 Ndipo Omri na Waisraeli wote pamoja
naye wakaondoka Gibethoni na kuizingira
Tirsa. 18 Wakati Zimri alipoona kuwa mji
umechukuliwa, alikwenda ndani ya ngome
ya jumba la kifalme na kulichoma moto
jumba la kifalme na kujiteketeza ndani
yake. Kwa hiyo akafa, 19 kwa sababu
ya dhambi alizofanya, akitenda maovu
machoni pa Bwana na kuenenda katika
njia za Yeroboamu na katika dhambi
alizofanya na kusababisha Israeli kuzifanya.
20 Kwa matukio mengine ya utawala wa
Zimri, na uasi alioutenda, je, hayakuandikwa
katika kitabu cha kumbukumbu za wafalme
wa Israeli?

*Omri Mfalme Wa Israeli*

21 Ndipo watu wa Israeli wakagawanyika
katika makundi mawili, nusu wakamuunga
mkono Tibni mwana wa Ginathi ili awe
mfalme na nusu nyingine wakamuunga
mkono Omri. 22 Lakini wafuasi wa Omri
wakajionyesha wenye nguvu kuliko wale
wa Tibni mwana wa Ginathi. Hivyo Tibni
akafa na Omri akawa mfalme.
23 [e]Katika mwaka wa thelathini na moja
wa utawala wa Asa mfalme wa Yuda, Omri
akawa mfalme wa Israeli, naye akatawala
kwa miaka kumi na miwili, sita kati ya
hiyo katika Tirsa. 24 [f]Alinunua kilima cha
Samaria kutoka kwa Shemeri kwa talanta
mbili[g] za fedha na akajenga mji juu ya
hicho kilima, akiuita Samaria, kutokana
na Shemeri, jina la mmiliki wa kwanza wa
kilima hicho.
25 [h]Lakini Omri akatenda maovu machoni
pa Bwana na kutenda dhambi kuliko wote
waliomtangulia. 26 [i]Akaenenda katika njia
zote za Yeroboamu mwana wa Nebati na
katika dhambi zake, ambazo alisababisha
Israeli kutenda, hivyo basi wakamkasirisha
Bwana, Mungu wa Israeli kwa sanamu zao
zisizofaa.
27 Kwa matukio mengine ya utawala
wa Omri, yale aliyofanya na vitu
alivyovifanikisha, je, hayakuandikwa katika
kitabu cha kumbukumbu za wafalme wa

[a]**16:9** 1Fal 20:12; Mit 31:4-5
[b]**16:10** 2Fal 9:31
[c]**16:13** Kum 32:21
[d]**16:15** Yos 19:44
[e]**16:23** Yos 12:24
[f]**16:24** 1Fal 13:32; Mt 10:5
[g]24 Talanta mbili za fedha ni sawa na kilo 70.
[h]**16:25** Kum 4:25; Mik 6:16
[i]**16:26** Kum 32:21

Israeli? 28 [a]Omri akalala pamoja na baba
zake na akazikwa huko Samaria. Ahabu
mwanawe akatawala mahali pake.

*Ahabu Afanywa Mfalme Wa Israeli*

29 Katika mwaka wa thelathini na nane
wa utawala wa Asa mfalme wa Yuda, Ahabu
mwana wa Omri akawa mfalme wa Israeli,
naye akatawala Israeli akiwa Samaria kwa
miaka ishirini na miwili. 30 [b]Ahabu mwana
wa Omri akafanya maovu zaidi machoni
mwa BWANA kuliko yeyote aliyewatangulia.
31 [c]Kama vile haikutosha kuishi kama
Yeroboamu mwana wa Nebati, akamwoa
Yezebeli binti wa Ethbaali, mfalme wa
Wasidoni, naye akaanza kumtumikia Baali
na kumwabudu. 32 [d]Akajenga madhabahu
kwa ajili ya Baali katika hekalu la Baali
lile alilolijenga huko Samaria. 33 [e]Pia Ahabu
akatengeneza nguzo ya Ashera na kufanya
mengi ili kumkasirisha BWANA, Mungu wa
Israeli, kuliko walivyofanya wafalme wote
wa Israeli waliomtangulia.

34 [f]Katika wakati wa Ahabu, Hieli,
Mbetheli, akaijenga upya Yeriko. Aliweka
misingi yake kwa gharama ya mzaliwa wake
wa kwanza Abiramu, na kuweka malango
yake kwa gharama ya mwanawe mdogo
Segubu, kulingana na neno la BWANA
alilosema kupitia Yoshua mwana wa Nuni.

*Eliya Analishwa Na Kunguru*

17 [g]Basi Eliya, Mtishbi kutoka Tishbi
katika Gileadi, akamwambia Ahabu,
"Kama BWANA, Mungu wa Israeli, aishivyo,
ambaye ninamtumikia, hapatakuwa na
umande wala mvua katika miaka hii,
isipokuwa kwa neno langu."

2 Kisha neno la BWANA likamjia Eliya,
kusema, 3 [h]"Ondoka hapa, elekea upande
wa mashariki ukajifiche katika Kijito
cha Kerithi, mashariki mwa Yordani.
4 [i]Utakunywa maji kutoka kile kijito, nami
nimeagiza kunguru wakulishe huko."

5 Hivyo akafanya kile alichoambiwa na
BWANA. Akaenda katika Kijito cha Kerithi,
mashariki ya Yordani na akakaa huko.
6 [j]Kunguru wakamletea mkate na nyama
asubuhi na mkate na nyama jioni, naye
akanywa maji kutoka kile kijito.

*Mjane Wa Sarepta*

7 Baada ya muda, kile kijito kikakauka
kwa sababu mvua haikuwa imenyesha
katika nchi. 8 Kisha neno la BWANA
likamjia, kusema, 9 [k]"Ondoka, uende Sarepta
ya Sidoni na ukae huko. Nimemwagiza
mjane katika sehemu ile akupatie chakula."
10 [l]Hivyo akaenda Sarepta. Alipofika kwenye
lango la mji, mjane alikuwa huko akiokota
kuni. Akamwita na kumwambia, "Naomba
uniletee maji kidogo kwenye gudulia ili
niweze kunywa." 11 Alipokuwa anakwenda
kumletea, akamwita akasema, "Tafadhali
niletee pia kipande cha mkate."

12 [m]Akamjibu, "Hakika kama BWANA
Mungu wako aishivyo, sina mkate wowote,
isipokuwa konzi ya unga kwenye gudulia na
mafuta kidogo kwenye chupa. Ninakusanya
kuni chache nipeleke nyumbani na nikapike
chakula kwa ajili yangu na mwanangu, ili
kwamba tule, kiishe, tukafe."

13 Eliya akamwambia, "Usiogope. Nenda
nyumbani ukafanye kama ulivyosema.
Lakini kwanza unitengenezee mimi mkate
mdogo kutoka vile ulivyo navyo kisha
uniletee na ndipo utayarishe chochote
kwa ajili yako na mwanao. 14 Kwa kuwa
hivi ndivyo asemavyo BWANA, Mungu wa
Israeli: 'Lile gudulia la unga halitakwisha
wala ile chupa ya mafuta haitakauka hadi
siku ile BWANA atakapoleta mvua juu ya
nchi.' "

15 Akaondoka na kufanya kama Eliya
alivyomwambia. Kwa hiyo kukawa na
chakula kila siku kwa ajili ya Eliya, yule
mwanamke na jamaa yake. 16 Kwa kuwa lile

---

[a]**16:28** 1Fal 13:32
[b]**16:30** 1Fal 14:9
[c]**16:31** 1Fal 11:2; 2Fal 9:34; Amu 3:6
[d]**16:32** Amu 6:28; Yer 43:12
[e]**16:33** Amu 3:7; 2Fal 13:6
[f]**16:34** Yos 6:26
[g]**17:1** Mal 4:5; Ay 12:15; Lk 4:25
[h]**17:3** 1Fal 18:4, 10; Yer 36:19, 26
[i]**17:4** Mwa 8:7
[j]**17:6** Kut 16:8
[k]**17:9** Oba 1:20; Lk 4:26
[l]**17:10** Mwa 24:17; Yn 4:7
[m]**17:12** 2Fal 4:2

gudulia la unga halikwisha na ile chupa ya
mafuta haikukauka, sawasawa na lile neno
la BWANA alilosema Eliya.
17 Baada ya muda, mwana wa yule
mwanamke mwenye nyumba akaugua.
Hali yake ikaendelea kuwa mbaya
sana, na hatimaye akaacha kupumua.
18 [a]Akamwambia Eliya, “Una nini dhidi
yangu, ewe mtu wa Mungu? Umekuja ili
kukumbushia dhambi yangu na kusababisha
kifo cha mwanangu?”
19 Eliya akamjibu, “Nipe mwanao.”
Eliya akampokea kutoka kifuani mwake,
akambeba mpaka chumba cha juu
alipokuwa anaishi, akamlaza kitandani
mwake. 20 [b]Kisha akamlilia BWANA, akasema
“Ee BWANA Mungu wangu, je, pia umeleta
msiba juu ya mjane huyu ninayeishi pamoja
naye, kwa kusababisha mwanawe kufa?”
21 [c]Kisha akajinyoosha juu ya kijana mara
tatu na kumlilia BWANA, akisema, “Ee
BWANA Mungu wangu, nakuomba roho
ya huyu kijana imrudie!”
22 BWANA akasikia kilio cha Eliya, na
roho ya kijana ikamrudia, naye akafufuka.
23 [d]Eliya akamtwaa kijana na kumbeba
kutoka chumbani mwake akamshusha
kumpeleka kwenye nyumba. Akampa mama
yake na kusema, “Tazama, mwanao yu hai!”
24 [e]Ndipo yule mwanamke akamwambia
Eliya, “Sasa ninajua kwamba wewe ni mtu
wa Mungu, na kwamba neno la BWANA
kutoka kinywani mwako ni kweli.”

### *Eliya Na Obadia*

18 [f]Baada ya muda mrefu, katika mwaka
wa tatu, neno la BWANA likamjia Eliya
kusema, “Nenda ukajionyeshe kwa Ahabu
na mimi nitanyesha mvua juu ya nchi.”
2 [g]Kwa hiyo Eliya akaenda kujionyesha
kwa Ahabu.
Wakati huu njaa ilikuwa kali sana katika
Samaria, 3 [h]naye Ahabu alikuwa amemwita
Obadia ambaye alikuwa msimamizi wa
jumba lake la kifalme. (Obadia alimcha
BWANA sana. 4 [i]Wakati Yezebeli alipokuwa
akiwaua manabii wa BWANA, Obadia
alikuwa amewachukua manabii mia moja
na kuwaficha katika mapango mawili,
hamsini kwenye kila moja na akawa
akiwapa chakula na maji.) 5 [j]Ahabu alikuwa
amemwambia Obadia, “Nenda katika nchi
yote kwenye vijito vyote na mabonde.
Huenda tunaweza kupata majani ya
kuwalisha farasi na nyumbu wapate kuishi
ili tusilazimike kuwaua hata mmoja wa
wanyama wetu.” 6 Kwa hiyo wakagawanya
nchi waliyokusudia kutafuta majani, Ahabu
akaenda upande mmoja na Obadia upande
mwingine.
7 [k]Wakati Obadia alipokuwa akitembea
njiani, Eliya akakutana naye. Obadia
akamtambua, akamsujudia hadi nchi na
kusema, “Je, hivi kweli ni wewe, bwana
wangu Eliya?”
8 Eliya akamjibu, “Ndiyo, nenda
ukamwambie bwana wako Ahabu, ‘Eliya
yuko hapa.’ ”
9 Obadia akamuuliza, “Ni kosa gani
nimefanya, hata ukaamua kumkabidhi
mtumishi wako mkononi mwa Ahabu ili
aniue? 10 [l]Hakika kama BWANA Mungu
wako aishivyo, hakuna taifa hata moja au
ufalme ambapo bwana wangu hajamtuma
mtu kukutafuta. Kila wakati taifa au ufalme
walipodai kwamba haupo huko, aliwafanya
waape kwamba hawakuweza kukupata.
11 Lakini sasa unaniambia niende kwa
bwana wangu na kusema, ‘Eliya yuko hapa.’
12 [m]Sijui ni wapi Roho wa BWANA ataamua
kukupeleka wakati nitakapokuacha. Kama
nikienda kumwambia Ahabu na asikupate,
ataniua. Hata hivyo mimi mtumishi wako
nimemwabudu BWANA tangu ujana wangu.
13 Je, hukusikia, bwana wangu, nilifanya
nini wakati Yezebeli alipokuwa akiua

[a]**17:18** Lk 5:8
[b]**17:20** 2Fal 4:33
[c]**17:21** 2Fal 4:34; Mdo 20:10
[d]**17:23** Ebr 11:35
[e]**17:24** Yn 16:30; Za 119:43
[f]**18:1** Lk 4:25; Kum 28:12
[g]**18:2** Law 26:26
[h]**18:3** 1Fal 16:9; Neh 7:2
[i]**18:4** 1Fal 21:23; Yer 26:24
[j]**18:5** Yer 14:3; Mwa 47:4
[k]**18:7** 2Fal 1:8; Zek 13:4
[l]**18:10** 1Fal 17:3
[m]**18:12** 2Fal 2:16; Eze 3:14; Mdo 8:39

manabii wa BWANA? Niliwaficha manabii
wa BWANA mia moja katika mapango
mawili, hamsini katika kila moja, nami
nikawapatia chakula na maji. [14] Nawe
sasa unaniambia niende kwa bwana wangu
na kumwambia, ‘Eliya yuko hapa.’ Yeye
ataniua!”
[15] Eliya akasema, “Kama BWANA Mwenye
Nguvu Zote aishivyo, yeye ninayemtumikia,
hakika nitajionyesha kwa Ahabu leo.”

*Eliya Juu Ya Mlima Karmeli*

[16] Basi Obadia akaenda kukutana na
Ahabu na kumwambia, naye Ahabu
akaenda kukutana na Eliya. [17] [a]Ahabu
alipomwona Eliya, akamwambia, “Je, ni
wewe, mtaabishaji wa Israeli?”
[18] [b]Eliya akamjibu, “Mimi sijaitaabisha
Israeli. Lakini wewe na jamaa ya baba yako
ndio mnaofanya hivyo. Mmeziacha amri
za BWANA na mkafuata Mabaali. [19] [c]Sasa
waite watu kutoka Israeli yote tukutane
nao juu ya Mlima Karmeli. Nawe uwalete
hao manabii wa Baali mia nne na hamsini
na hao manabii mia nne wa Ashera, walao
chakula mezani mwa Yezebeli.”
[20] [d]Ndipo Ahabu akatuma ujumbe katika
Israeli yote na kuwakusanya manabii hao
juu ya mlima Karmeli. [21] [e]Eliya akasimama
mbele ya watu na kusema, “Mtasitasita
katika mawazo mawili hadi lini? Ikiwa
BWANA ndiye Mungu, mfuateni yeye; lakini
ikiwa Baali ni Mungu, basi mfuateni yeye.”
Lakini watu hawakusema kitu.
[22] [f]Kisha Eliya akawaambia, “Ni mimi
peke yangu nabii wa BWANA aliyebaki,
lakini Baali ana manabii mia nne na
hamsini. [23] Leteni mafahali wawili. Wao
na wajichagulie mmoja, wamkate vipande
vipande na waweke juu ya kuni lakini
wasiiwashie moto. Nitamwandaa huyo
fahali mwingine na kumweka juu ya kuni
lakini sitawasha moto. [24] [g]Kisha mliitie
jina la mungu wenu, nami nitaliitia jina la
BWANA Mungu yule ambaye atajibu kwa
moto, huyo ndiye Mungu.”
Kisha watu wote wakasema, “Hilo
unalosema ni jema.”
[25] Eliya akawaambia manabii wa Baali,
“Chagueni mmoja kati ya hawa mafahali
na mwe wa kwanza kumwandaa, kwa kuwa
ninyi mko wengi sana. Liitieni jina la mungu
wenu, lakini msiwashe moto.” [26] [h]Kwa hiyo
wakamchukua yule fahali waliyepewa, nao
wakamwandaa.
Kisha wakaliitia jina la Baali kutoka
asubuhi hadi adhuhuri, wakapiga kelele,
“Ee Baali, utujibu!” Lakini hapakuwa na
jibu; hakuna aliyejibu. Nao wakacheza
kuizunguka madhabahu waliyoijenga.
[27] Wakati wa adhuhuri, Eliya akaanza
kuwadhihaki, akisema, “Pigeni kelele zaidi!
Hakika yeye ni mungu! Labda amezama
katika mawazo mazito, au ana shughuli
nyingi, au amesafiri. Labda amelala
usingizi mzito, naye ni lazima aamshwe.”
[28] [i]Kwa hiyo wakapiga kelele zaidi na
kama ilivyokuwa desturi yao wakajichanja
wenyewe kwa visu na vyembe, mpaka
damu ikachuruzika. [29] [j]Adhuhuri ikapita,
nao wakaendelea na utabiri wao wa
kiwazimu mpaka wakati wa dhabihu ya
jioni. Lakini hapakuwa na jibu, hakuna
aliyejibu, hakuna aliyeangalia.
[30] [k]Kisha Eliya akawaambia watu
wote, “Sogeeni karibu nami.” Watu
wote wakamkaribia, naye akakarabati
madhabahu ya BWANA, ambayo ilikuwa
imevunjwa. [31] [l]Eliya akachukua mawe kumi
na mawili, moja kwa ajili ya kila kabila la
wana wa Yakobo, ambaye neno la BWANA
lilimjia, likisema, “Jina lako litakuwa
Israeli.” [32] [m]Kwa mawe hayo, akajenga
madhabahu katika jina la BWANA, na
akachimba handaki kuizunguka, ukubwa
wa kutosha vipimo viwili vya mbegu.

---

[a]**18:17** Yos 7:25; 1Fal 21:20
[b]**18:18** 1Fal 16:33
[c]**18:19** 2Fal 10:19; Yos 19:26
[d]**18:20** 2Fal 2:25; 4:25
[e]**18:21** Yos 24:15; 2Fal 17:41; Mt 6:24
[f]**18:22** 1Fal 19:10; Yer 2:8
[g]**18:24** 1Sam 7:8; Law 9:24
[h]**18:26** Za 115:4-5; 1Kor 8:4; 12:2
[i]**18:28** Law 19:28
[j]**18:29** Kut 29:41; 2Fal 19:12; Isa 16:12
[k]**18:30** 1Fal 19:10
[l]**18:31** 2Fal 17:34; Mwa 17:5
[m]**18:32** Kol 3:17; Kum 18:7

[33] [a]Akapanga kuni, akamkata yule fahali
vipande vipande na kuvipanga juu ya
kuni. Kisha akawaambia, "Jazeni mapipa
manne maji na kuyamwaga juu ya sadaka
ya kuteketezwa na juu ya kuni."
[34] Akawaambia, "Fanyeni hivyo tena."
Nao wakafanya hivyo tena.
Akaagiza, "Fanyeni kwa mara ya tatu."
Nao wakafanya hivyo kwa mara ya tatu.
[35] Maji yakatiririka kuizunguka madhabahu
na hata kujaza lile handaki.
[36] [b]Wakati wa kutoa dhabihu ya jioni, nabii
Eliya akasogea mbele na kuomba, akisema:
"Ee Bwana, Mungu wa Abrahamu, na Isaki
na Israeli, ijulikane leo kwamba wewe ndiye
Mungu katika Israeli na ya kwamba mimi ni
mtumishi wako na nimefanya mambo haya
yote kwa neno lako. [37] [c]Unijibu mimi, Ee
Bwana, nijibu mimi, ili watu hawa wajue
kwamba wewe, Ee Bwana, ndiwe Mungu,
na kwamba unaigeuza mioyo yao ikurudie
tena."
[38] [d]Kisha moto wa Bwana ukashuka na
kuiteketeza ile dhabihu, zile kuni, yale
mawe, ule udongo, na pia kuramba yale
maji yaliyokuwa ndani ya handaki.
[39] [e]Wakati watu wote walipoona hili,
wakaanguka kifudifudi na kulia, "Bwana:
yeye ndiye Mungu! Bwana: yeye ndiye
Mungu!"
[40] [f]Kisha Eliya akawaamuru, "Wakamateni
hao manabii wa Baali. Msimwache hata
mmoja atoroke!" Wakawakamata, naye
Eliya akawaleta mpaka Bonde la Kishoni
na kuwachinja huko.
[41] Eliya akamwambia Ahabu, "Nenda,
ukale na kunywa, kwa kuwa kuna sauti ya
mvua kubwa." [42] [g]Hivyo Ahabu akaondoka
ili kula na kunywa. Lakini Eliya akapanda
kileleni mwa Karmeli, akasujudu na
akaweka kichwa chake katikati ya magoti
yake.
[43] Akamwambia mtumishi wake, "Nenda
ukatazame kuelekea bahari." Akaenda na
kutazama.
Akasema, "Hakuna kitu chochote huko."
Mara saba Eliya akasema, "Nenda tena."
[44] [h]Mara ya saba, mtumishi akaleta
taarifa, "Wingu dogo kama mkono wa
mwanadamu linainuka kutoka baharini."
Hivyo Eliya akasema, "Nenda
ukamwambie Ahabu, 'Tandika gari lako
na ushuke kabla mvua haijakuzuia.' "
[45] [i]Wakati ule ule anga likawa jeusi
kwa mawingu, upepo ukainuka na mvua
kubwa ikanyesha, naye Ahabu akaenda
zake Yezreeli. [46] [j]Nguvu za Bwana zikamjia
Eliya, naye akajikaza viuno, akakimbia
mbele ya Ahabu njia yote hadi maingilio
ya Yezreeli.

### *Eliya Akimbilia Horebu*

19 [k]Ahabu akamwambia Yezebeli kila kitu
Eliya alichokuwa amefanya na jinsi
alivyowaua manabii wote kwa upanga.
[2] [l]Hivyo Yezebeli akamtuma mjumbe kwa
Eliya, kusema, "Hao miungu initendee hivyo
na kuzidi, kama kufikia kesho wakati kama
huu sitaifanya roho yako kama mmojawapo
wa hao manabii."
[3] [m]Eliya aliogopa, na akakimbia kuokoa
maisha yake. Alipofika Beer-Sheba katika
Yuda, akamwacha mtumishi wake huko,
[4] [n]lakini yeye mwenyewe akatembea
mwendo wa kutwa nzima katika jangwa.
Akafika kwenye mti wa mretemu, akakaa
chini yake na kuomba ili afe. Akasema,
"Yatosha sasa, Bwana, ondoa roho yangu,
kwani mimi si bora kuliko baba zangu."
[5] [o]Kisha akajinyoosha chini ya mti, akalala
usingizi.
Mara malaika akamgusa na akamwambia,
"Inuka na ule." [6] Akatazama pande zote,
napo hapo karibu na kichwa chake
palikuwepo mkate uliookwa kwenye

[a]**18:33** Mwa 22:9
[b]**18:36** Kut 29:39, 41; Yos 4:24; Hes 16:28
[c]**18:37** Yos 4:24
[d]**18:38** Law 9:24; 1Nya 21:26; Ay 1:16
[e]**18:39** Law 9:24; Za 46:10
[f]**18:40** Amu 4:7; Kut 22:20
[g]**18:42** Yak 5:18; Isa 5:18
[h]**18:44** Yos 6:15; Lk 12:54
[i]**18:45** Ay 37:13; Hos 1:4
[j]**18:46** Amu 3:10; 2Fal 4:29
[k]**19:1** 1Fal 16:31; Kut 22:20
[l]**19:2** Rut 1:17; Za 13:4
[m]**19:3** Mwa 31:21; Yos 19:2
[n]**19:4** Hes 11:15; Yon 4:8
[o]**19:5** Mwa 28:11

makaa ya moto na gudulia la maji. Akala
na kunywa, kisha akajinyoosha tena.
7 Yule malaika wa BWANA akaja tena
mara ya pili, akamgusa akamwambia,
"Inuka na ule, kwa kuwa safari ni ndefu
kwako." 8 [a]Kwa hiyo akainuka, akala na
kunywa. Akiwa ametiwa nguvu na kile
chakula, akasafiri siku arobaini usiku na
mchana mpaka akafika Horebu, mlima
wa Mungu. 9 Huko akaingia katika pango,
akalala humo usiku ule.

*BWANA Amtokea Eliya*

Nalo neno la BWANA likamjia, kusema,
"Unafanya nini hapa, Eliya?"
10 [b]Akajibu, "Nimeona wivu mwingi kwa
ajili ya BWANA Mungu Mwenye Nguvu
Zote. Waisraeli wamelikataa Agano lako,
wamevunja madhabahu zako na kuwaua
manabii wako kwa upanga. Ni mimi,
mimi peke yangu, niliyebaki, nao sasa
wananitafuta ili waniangamize." 11 [c]BWANA
akasema, "Toka nje ukasimame juu ya
mlima mbele za BWANA, kwa kuwa BWANA
yu karibu kupita hapo."
Kisha upepo mwingi na wenye nguvu
ukapasua milima ile na kuvunjavunja
miamba mbele za BWANA, lakini BWANA
hakuwamo katika ule upepo. Baada ya
upepo palikuwa na tetemeko la nchi, lakini
BWANA hakuwamo kwenye lile tetemeko.
12 [d]Baada ya tetemeko la nchi ukaja moto,
lakini BWANA hakuwamo katika ule moto.
Baada ya moto ikaja sauti ya utulivu ya
kunong'ona. 13 [e]Eliya alipoisikia, akafunika
uso kwa vazi lake, akatoka na kusimama
kwenye mdomo wa pango.
Kisha ile sauti ikamwambia, "Eliya,
unafanya nini hapa?"
14 Akajibu, "Nimeona wivu mwingi kwa
ajili ya BWANA Mungu Mwenye Nguvu
Zote. Waisraeli wamelikataa Agano lako,
wamevunja madhabahu zako na kuwaua
manabii wako kwa upanga. Ni mimi,
mimi peke yangu, niliyebaki, nao sasa
wananitafuta ili waniangamize."
15 [f]BWANA akamwambia, "Rudi kwa njia
uliyoijia, uende kwenye Jangwa la Dameski.
Wakati utakapofika huko, mtie Hazaeli
mafuta awe mfalme wa Aramu[g] 16 Pia
mtie mafuta Yehu mwana wa Nimshi awe
mfalme wa Israeli, na umtie Elisha mwana
wa Shafati kutoka Abel-Mehola mafuta awe
nabii badala yako. 17 [h]Yehu atamuua yeyote
atakayeutoroka upanga wa Hazaeli, naye
Elisha atamuua yeyote atakayeutoroka
upanga wa Yehu. 18 [i]Hata sasa nimeweka
akiba watu elfu saba katika Israeli, wote
ambao hawajampigia Baali magoti, na wote
ambao midomo yao haijambusu."

*Wito Wa Elisha*

19 Hivyo Eliya akaondoka kutoka huko
na kumkuta Elisha mwana wa Shafati.
Alikuwa akilima kwa jozi kumi na mbili
za maksai, na yeye mwenyewe aliongoza ile
jozi ya kumi na mbili. Eliya akapita karibu
naye, akamrushia vazi lake. 20 [j]Kisha Elisha
akawaacha maksai wake, akamkimbilia
Eliya, akamwambia, "Niruhusu nikawabusu
baba yangu na mama yangu, halafu
nitafuatana nawe."
Eliya akajibu, "Rudi zako, kwani
nimekutendea nini?"
21 Basi Elisha akamwacha Eliya, naye
akarudi. Akachukua ile jozi yake ya maksai
na kuwachinja. Akaipika ile nyama kwa
kutumia miti ya nira kama kuni na kuwapa
watu, nao wakala. Kisha akaondoka,
akamfuata Eliya, akamtumikia.

*Ben-Hadadi Aishambulia Samaria*

20 [k]Wakati huu, Ben-Hadadi mfalme
wa Aramu akakusanya jeshi lake
lote. Akifuatana na wafalme thelathini
na wawili wakiwa na farasi na magari
ya vita, akakwea kuuzingira kwa jeshi
Samaria na kuishambulia. 2 Akawatuma

[a]**19:8** Kut 3:1; Mt 4:2
[b]**19:10** 1Fal 18:30; Rum 11:3
[c]**19:11** Kut 34:2; Nah 1:6
[d]**19:12** Kut 3:2; 1Sam 14:6; Ay 4:16
[e]**19:13** Kut 3:6
[f]**19:15** 2Fal 8:7-15
[g]15 Yaani Shamu (ambayo leo ni Syria).
[h]**19:17** 2Fal 8:12, 29; Yer 48:44
[i]**19:18** Rum 11:4; Hos 13:2
[j]**19:20** Lk 9:61
[k]**20:1** 1Fal 15:18; 13:32

wajumbe katika mji kwa Ahabu mfalme
wa Israeli, kusema, “Hivi ndivyo asemavyo
Ben-Hadadi: 3 ‘Fedha yako na dhahabu ni
yangu, nao wake zako walio wazuri sana
na watoto ni wangu.’ ”

4 Mfalme wa Israeli akajibu, “Iwe kama
usemavyo, bwana wangu mfalme. Mimi na
vyote nilivyo navyo ni mali yako.”

5 Wale wajumbe wakaja tena na kusema,
“Hivi ndivyo asemavyo Ben-Hadadi:
‘Nimetuma kutaka fedha yako na dhahabu,
wake zako na watoto wako. 6 Lakini kesho
wakati kama huu, nitawatuma maafisa
wangu kukagua jumba lako la kifalme na
nyumba za maafisa wako. Watatwaa kitu
unachokithamini nao watakichukua.’ ”

7 [a]Mfalme wa Israeli akawaita wazee
wote wa nchi na akawaambia, “Tazama
jinsi mtu huyu anavyochokoza! Wakati
alipotuma apelekewe wake zangu na watoto
wangu, fedha zangu na dhahabu yangu,
sikumkatalia.”

8 Wazee na watu wote wakajibu,
“Usimsikilize, wala usiyakubali matakwa
yake.”

9 Kwa hiyo akawajibu wajumbe wa
Ben-Hadadi, “Mwambieni bwana wangu
mfalme, ‘Mtumishi wako atafanya yote
uliyoyadai mwanzoni, lakini dai hili la
sasa siwezi kulitekeleza.’ ” Wakaondoka
na kupeleka jibu kwa Ben-Hadadi.

10 [b]Kisha Ben-Hadadi akatuma ujumbe
mwingine kwa Ahabu, kusema “Miungu
iniletee maafa, tena makubwa zaidi, ikiwa
vumbi la Samaria litatosheleza konzi moja
ya kila mtu ya wale wafuatanao nami.”

11 [c]Mfalme wa Israeli akajibu,
“Mwambieni, ‘Yule anayevaa mavazi ya
vita asije akajisifu kama yule anayevua.’ ”

12 [d]Ben-Hadadi alisikia ujumbe huu
wakati ambapo yeye na wafalme walikuwa
wanakunywa katika mahema yao, na
akawaamuru watu wake, “Jiandaeni
kushambulia.” Kwa hiyo wakajiandaa
kuushambulia mji.

*Ahabu Amshinda Ben-Hadadi*

13 [e]Wakati ule ule nabii akamjia Ahabu
mfalme wa Israeli na kutangaza, “Hivi
ndivyo asemavyo BWANA: ‘Je, unaona jeshi
hili kubwa? Nitalitia mkononi mwako leo,
nawe ndipo utajua kwamba mimi ndimi
BWANA.’ ”

14 [f]Ahabu akauliza, “Ni nani atakayefanya
hili?”

Nabii akamjibu, “Hivi ndivyo asemavyo
BWANA: ‘Maafisa vijana majemadari wa
majimbo watafanya hili.’ ”

Akauliza, “Ni nani atakayeanzisha vita?”

Nabii akamjibu, “Ni wewe.”

15 Kwa hiyo Ahabu akawaita maafisa
vijana majemadari wa majimbo, wanaume
232. Kisha akawakusanya Waisraeli wote
waliobaki, jumla yao 7,000. 16 [g]Wakaondoka
wakati wa adhuhuri, Ben-Hadadi na wale
wafalme thelathini na wawili walioungana
naye walipokuwa katika mahema yao
wakilewa. 17 Maafisa vijana majemadari
wa majimbo waliondoka kwanza.

Wakati huu Ben-Hadadi alikuwa
amewatuma wapelelezi, ambao walileta
taarifa kusema kwamba, “Askari wanasonga
mbele kutoka Samaria.”

18 Akasema, “Ikiwa wamekuja kwa amani,
wakamate wakiwa hai; ikiwa wamekuja
kwa vita, wakamate wakiwa hai.”

19 Wale maafisa vijana majemadari wa
majimbo wakatoka nje ya mji jeshi likiwa
nyuma yao, 20 kila mmoja akamuua adui
yake. Hii ilisababisha Waaramu kukimbia,
huku Waisraeli wakiwafuatia. Lakini Ben-
Hadadi mfalme wa Aramu akatoroka akiwa
amepanda farasi wake pamoja na baadhi
ya wapanda farasi wake. 21 Mfalme wa
Israeli akasonga mbele na kushinda farasi
na magari ya vita na kusababisha hasara
kubwa kwa Waaramu.

22 [h]Baadaye nabii akaja kwa mfalme wa
Israeli na kusema, “Jiandae vizuri ufikirie
la kufanya, kwa sababu mwakani mfalme
wa Aramu atakuja kukushambulia tena.”

23 Wakati ule ule, maafisa wa mfalme

[a]**20:7** 1Sam 11:3; 2Fal 5:7
[b]**20:10** 2Sam 22:43
[c]**20:11** Mit 27:1; Amo 2:14
[d]**20:12** 1Fal 16:9; 20:13
[e]**20:13** Amu 6:8; Kut 6:7
[f]**20:14** Amu 1:1
[g]**20:16** 1Fal 16:9
[h]**20:22** 2Sam 11:1

wa Aramu wakamshauri, wakamwambia,
“Miungu yao ni miungu ya vilimani.
Ndiyo sababu walikuwa na nguvu sana
kutuzidi. Lakini kama tukipigana nao katika
nchi tambarare, hakika tutawashinda.
24 Fanya hivi: Waondoe hao wafalme wote
thelathini na wawili kutoka nafasi zao na
uweke maafisa wengine mahali pao. 25 Ni
lazima pia uandae jeshi jingine kama lile
ulilopoteza, farasi kwa farasi, gari la vita
kwa gari la vita, ili tuweze kupigana na
Israeli katika nchi tambarare. Kisha kwa
hakika tutakuwa na nguvu kuliko wao.”
Akakubaliana nao naye akashughulika
ipasavyo.

26 [a]Mwaka uliofuata, majira kama hayo,
Ben-Hadadi akawakusanya Waaramu
mpaka Afeki kupigana dhidi ya Israeli.
27 [b]Baada ya Waisraeli kukusanywa na
kupewa mahitaji, walikwenda kukabiliana
nao. Waisraeli wakapiga kambi mkabala
nao kama makundi mawili madogo ya
mbuzi, wakati Waaramu walienea katika
nchi yote.

28 [c]Mtu wa Mungu akaja na kumwambia
mfalme wa Israeli, “Hivi ndivyo BWANA
asemavyo: ‘Kwa sababu Waaramu
wanafikiri BWANA ni Mungu wa vilimani
na sio Mungu wa mabondeni, nitatia jeshi
hili kubwa mkononi mwako, nawe utajua
kuwa mimi ndimi BWANA.’ ”

29 Kwa siku saba walipiga kambi
wakitazamana na siku ya saba vita
vikaanza. Waisraeli wakawajeruhi askari
wa miguu wa Waaramu 100,000 kwa siku
moja. 30 [d]Waliobaki wakatorokea katika
mji wa Afeki, mahali ambapo watu 27,000
waliangukiwa na ukuta. Naye Ben-Hadadi
akakimbilia mjini na kujificha kwenye
chumba cha ndani.

31 [e]Maafisa wake wakamwambia,
“Tazama, tumesikia kwamba wafalme
wa nyumba ya Israeli wana huruma.
Twendeni kwa mfalme wa Israeli tukiwa
tumevaa nguo za gunia viunoni mwetu na
kamba kuzunguka vichwa vyetu. Huenda
akakuacha hai.”

32 Wakiwa wamevaa nguo za gunia
viunoni mwao na kamba kuzunguka vichwa
vyao, walikwenda kwa mfalme wa Israeli
na kusema, “Mtumishi wako Ben-Hadadi
anasema: ‘Tafadhali, naomba uniache hai.’ ”

Mfalme akajibu, “Je, bado yuko hai?
Yeye ni ndugu yangu.”

33 Wale watu wakalipokea jambo lile
kama dalili nzuri nao wakawa wepesi
kulichukua neno lake wakisema, “Ndiyo,
yeye ni ndugu yako Ben-Hadadi!”

Mfalme akawaambia, “Nendeni
mkamlete.” Ikawa Ben-Hadadi alipokuja,
Ahabu akampandisha katika gari lake la
vita.

Ben-Hadadi akajitolea, akisema,
34 [f]“Nitairudisha ile miji ambayo baba yangu
aliiteka kutoka kwa baba yako. Unaweza
kuweka maeneo yako ya soko katika
Dameski, kama baba yangu alivyofanya
huko Samaria.”

Ahabu akasema, “Katika misingi ya
mkataba, nitakuachilia huru.” Kwa hiyo
akaweka mkataba naye, akamruhusu aende
zake.

### *Nabii Amlaumu Ahabu*

35 [g]Kwa neno la BWANA, mmoja wa wana
wa manabii akamwambia mwenzake,
“Nipige kwa silaha yako,” lakini yule mtu
akakataa.

36 [h]Kwa hiyo yule nabii akasema,
“Kwa sababu hukumtii BWANA, mara
tu tutakapoachana utauawa na simba.”
Na baada ya yule mtu kuondoka, simba
akatokea na kumuua.

37 Nabii akamkuta mtu mwingine na
kumwambia, “Nipige tafadhali.” Kisha
yule mtu akampiga na kumjeruhi. 38 Ndipo
nabii akaenda na kusimama barabarani
akimsubiri mfalme. Akajibadilisha kwa
kushusha kitambaa cha kichwani mwake
hadi kwenye macho. 39 [i]Mfalme alipopita
pale, yule nabii akamwita, “Mtumishi

[a]**20:26** 2Fal 13:17
[b]**20:27** Amu 6:6; 1Sam 13:6
[c]**20:28** Kut 6:7; Yer 16:19-21
[d]**20:30** 1Fal 22:25; Za 62:4
[e]**20:31** Ay 41:3; Mwa 37:34
[f]**20:34** 1Fal 15:20; Kut 23:32
[g]**20:35** 1Sam 10:5; 1Fal 13:21
[h]**20:36** 1Fal 13:24
[i]**20:39** Yos 2:14

wako alikwenda vitani wakati vita
vilipopamba moto, mtu mmoja akanijia
na mateka akasema, ‘Mlinde mtu huyu.
Kama akitoroka itakuwa uhai wako kwa
uhai wake, ama vipande 3,000 vya fedha.’
40 [a]Wakati mtumishi wako alipokuwa na
shughuli nyingi hapa na pale, yule mtu
akatoweka.”

Mfalme wa Israeli akasema, “Hiyo ndiyo
hukumu yako. Wewe umeitaja mwenyewe.”

41 Kisha yule nabii akajifunua macho yake
haraka, na mfalme wa Israeli akamtambua
kama mmoja wa manabii. 42 [b]Akamwambia
mfalme, “Hivi ndivyo BWANA asemavyo:
‘Umemwacha huru mtu niliyekusudia afe.
Kwa hiyo ni uhai wako kwa uhai wake, watu
wako kwa watu wake.’ ” 43 [c]Kwa uchungu na
hasira, mfalme wa Israeli akaenda kwenye
jumba lake la kifalme huko Samaria.

*Shamba La Mizabibu La Nabothi*

21 [d]Baada ya hayo, Nabothi, Myezreeli,
alikuwa na shamba la mizabibu jirani
na jumba la kifalme la Ahabu mfalme wa
Samaria. 2 Ahabu akamwambia Nabothi,
“Nipe shamba lako la mizabibu nilitumie
kwa bustani ya mboga, kwa kuwa liko
karibu na jumba langu la kifalme. Badala
yake, nitakupa shamba jingine la mizabibu
zuri zaidi au, kama utapenda, nitakulipa
kiasi chochote unachoona ni thamani yake.”

3 [e]Lakini Nabothi akamjibu, “BWANA na
apishe mbali kukupa wewe urithi wa baba
zangu.”

4 [f]Basi Ahabu akaenda nyumbani,
mwenye huzuni na hasira kwa sababu ya
yale ambayo Nabothi, Myezreeli, alikuwa
amesema, “Sitakupa urithi wa baba zangu.”
Akajinyoosha juu ya kitanda akisononeka,
na akakataa kula.

5 Yezebeli mke wake akaingia na
akamuuliza, “Kwa nini unahuzunika hivi?
Kwa nini huli chakula?”

6 Akamjibu, “Kwa sababu nilimwambia
Nabothi, Myezreeli, ‘Niuzie shamba lako
la mizabibu, au kama ukipenda, nitakupa
shamba jingine la mizabibu badala yake.’
Lakini akasema, ‘Sitakupa shamba langu
la mizabibu.’ ”

7 [g]Yezebeli mke wake akasema, “Hivi
ndivyo unavyofanya, nawe ni mfalme katika
Israeli yote? Inuka na ule! Changamka.
Nitakupatia shamba la mizabibu la Nabothi,
Myezreeli.”

8 [h]Kwa hiyo akaandika barua kwa jina la
Ahabu akaweka muhuri wake juu ya hizo
barua, akazipeleka kwa wazee na kwa watu
wenye cheo walioishi katika mji pamoja
na Nabothi. 9 Katika barua hizo aliandika:

> “Tangazeni siku ya watu kufunga
> na mkamketishe Nabothi mahali pa
> wazi miongoni mwa watu. 10 [i]Lakini
> waketisheni watu wawili wabaya
> kabisa mkabala naye, nao washuhudie
> kuwa yeye amemlaani Mungu na
> mfalme. Kisha mtoeni nje na kumpiga
> kwa mawe hadi afe.”

11 Hivyo wazee na watu wenye cheo
walioishi katika mji wa Nabothi wakafanya
kama Yezebeli alivyoelekeza katika barua
aliyowaandikia. 12 [j]Wakatangaza mfungo
na kumketisha Nabothi mahali pa wazi
miongoni mwa watu. 13 [k]Kisha watu
wawili wabaya kabisa wakaja wakaketi
mkabala naye, nao wakaleta mashtaka
dhidi ya Nabothi mbele ya watu, wakisema,
“Nabothi amemlaani Mungu na mfalme.”
Kwa hiyo wakamtoa nje na kumpiga kwa
mawe hadi akafa. 14 Kisha wakatuma
ujumbe kwa Yezebeli, kusema, “Nabothi
amepigwa mawe na amekufa.”

15 [l]Mara tu Yezebeli aliposikia kwamba
Nabothi amepigwa mawe na amekufa,
akamwambia Ahabu, “Amka na uchukue lile
shamba la mizabibu la Nabothi, Myezreeli,
ambalo alikataa kukuuzia. Hayuko hai
tena, bali amekufa.” 16 Ahabu aliposikia

[a]**20:40** 2Sam 12:5
[b]**20:42** 2Sam 12:7; Yer 48:10
[c]**20:43** 1Fal 21:4
[d]**21:1** 2Fal 9:21; 1Sam 29:1
[e]**21:3** Law 25:23
[f]**21:4** 1Fal 20:43; Isa 28:23
[g]**21:7** 1Sam 8:14
[h]**21:8** Mwa 38:18
[i]**21:10** Kut 22:28; Law 24:15-16; Mdo 6:11
[j]**21:12** Isa 58:4
[k]**21:13** Law 24:16
[l]**21:15** 1Sam 8:14

Nabothi amekufa, akainuka na kushuka ili
kulichukua shamba la mizabibu la Nabothi.
17 Kisha neno la BWANA likamjia Eliya,
Mtishbi: 18 “Shuka ukakutane na Ahabu
mfalme wa Israeli, anayetawala Samaria.
Sasa yuko katika shamba la mizabibu la
Nabothi, ambapo amekwenda alimiliki.
19 [a]Umwambie, ‘Hivi ndivyo BWANA
asemavyo: Je, hujamuua mtu na kuitwaa
mali yake?’ Kisha umwambie, ‘Hivi ndivyo
asemavyo BWANA: Mahali ambapo mbwa
waliramba damu ya Nabothi, mbwa
watairamba damu yako, naam, yako
wewe!’ ”
20 [b]Ahabu akamwambia Eliya, “Kwa hiyo
umenipata, wewe adui yangu!”
Akajibu, “Ndiyo, nimekupata. Kwa
sababu umejiuza mwenyewe kufanya uovu
mbele ya macho ya BWANA. 21 ‘Nitaleta
maafa juu yako. Nitaangamiza uzao wako
na kukatilia mbali kutoka kwa Ahabu kila
mzaliwa wa mwisho wa kiume katika
Israeli, wa mtumwa au wa mtu huru.
22 [c]Nitaifanya nyumba yako kama ile ya
Yeroboamu mwana wa Nebati na ile ya
Baasha mwana wa Ahiya, kwa sababu
umenighadhibisha kwa kuwa umesababisha
Israeli kutenda dhambi.’
23 [d]“Pia kwa habari ya Yezebeli BWANA
anasema, ‘Mbwa watamla Yezebeli karibu
na ukuta wa Yezreeli.’
24 [e]“Mbwa watawala wale wa nyumba
ya Ahabu watakaofia mjini, nao wale
watakaofia mashambani wataliwa na ndege
wa angani.”
25 (Hapajapata kamwe kuwa na mtu kama
Ahabu, aliyejiuza mwenyewe kutenda uovu
machoni mwa BWANA, akiwa anachochewa
na Yezebeli mkewe. 26 [f]Alitenda kwa uovu
sana katika kuabudu sanamu, kama wale
Waamori ambao BWANA aliowafukuza
mbele ya Israeli.)
27 [g]Ahabu aliposikia maneno haya,
akararua nguo zake, akavaa nguo za gunia
na kufunga. Akalala na kujifunika nguo za
gunia na kwenda kwa unyenyekevu.
28 Ndipo neno la BWANA lilipomjia Eliya
Mtishbi kusema, 29 [h]“Umeona jinsi Ahabu
alivyojinyenyekeza mbele zangu? Kwa
kuwa amejishusha mwenyewe, sitaleta
maafa haya wakati akiwa hai, lakini
nitayaleta juu ya nyumba yake katika siku
za mwanawe.”

*Mikaya Anatabiri Dhidi Ya Ahabu*

**(2 Nyakati 18:2-27)**

22 Kwa miaka mitatu hapakuwa na vita
kati ya Aramu na Israeli. 2 Lakini
katika mwaka wa tatu Yehoshafati mfalme
wa Yuda akashuka kwenda kumwona
mfalme wa Israeli. 3 [i]Mfalme wa Israeli
alikuwa amewaambia maafisa wake, “Je,
hamjui Ramoth-Gileadi ni mali yetu na
bado hatufanyi chochote kuirudisha kwetu
kutoka kwa mfalme wa Aramu?”
4 [j]Kwa hiyo akamuuliza Yehoshafati, “Je,
utakwenda pamoja nami kupigana dhidi ya
Ramoth-Gileadi?”
Yehoshafati akamjibu mfalme wa Israeli,
“Mimi ni kama wewe, watu wangu ni
kama watu wako, farasi wangu ni kama
farasi wako.” 5 [k]Lakini Yehoshafati pia
akamwambia mfalme wa Israeli, “Kwanza
tafuta shauri la BWANA.”
6 [l]Kwa hiyo mfalme wa Israeli akawaleta
pamoja manabii wanaume wapatao mia
nne, akawauliza, “Je, niende vitani dhidi
ya Ramoth-Gileadi, au niache?”
Wakajibu, “Naam, nenda, kwa kuwa
Bwana ataiweka Ramoth-Gileadi mkononi
mwa mfalme.”
7 [m]Lakini Yehoshafati akauliza, “Je,
hayuko nabii wa BWANA hapa ambaye
tunaweza kumuuliza?”
8 [n]Mfalme wa Israeli akamjibu Yehoshafati,
“Bado yupo mtu mmoja ambaye kupitia

[a]**21:19** Ay 24:6; 1Fal 22:38
[b]**21:20** 1Fal 18:17; Rum 7:14
[c]**21:22** 1Fal 16:3
[d]**21:23** 2Fal 9:10, 34-36
[e]**21:24** 1Fal 14:11; Mwa 40:19
[f]**21:26** Mwa 15:16
[g]**21:27** Mwa 37:34; Yer 4:8; Isa 38:15
[h]**21:29** Kut 32:14; 2Fal 9:26
[i]**22:3** Kum 4:43
[j]**22:4** 2Fal 3:7
[k]**22:5** Kut 33:7; Ay 38:2; 2Fal 3:11
[l]**22:6** Amu 18:6
[m]**22:7** Hes 27:21; 2Fal 3:11
[n]**22:8** Amo 5:10; Yer 23:17

yeye twaweza kumuuliza shauri la BWANA,
lakini namchukia kwa sababu huwa hatabiri
jambo lolote jema kunihusu mimi, lakini
kila mara hunitabiria mabaya tu. Yeye ni
Mikaya mwana wa Imla."

Yehoshafati akajibu, "Mfalme hapaswi
kusema hivyo."

9 Kwa hiyo mfalme wa Israeli akamwita
mmoja wa maafisa wake na kusema, "Mlete
Mikaya mwana wa Imla mara moja."

10 Wakiwa wamevalia majoho yao ya
kifalme, mfalme wa Israeli na Yehoshafati
mfalme wa Yuda walikuwa wameketi juu
ya viti vyao vya kifalme katika sakafu ya
kupuria, kwenye ingilio la lango la Samaria,
pamoja na manabii wote wakiwa wakitabiri
mbele yao. 11 [a]Wakati huu Sedekia mwana
wa Kenaana alikuwa ametengeneza pembe
za chuma, akatangaza, "Hivi ndivyo BWANA
asemavyo, 'Kwa hizi pembe utawapiga na
kuwarudisha Waaramu nyuma mpaka
wameangamizwa.' "

12 Manabii wengine wote walikuwa
wanatabiri kitu hicho hicho wakisema,
"Ishambulie Ramoth-Gileadi na uwe
mshindi. Kwa kuwa BWANA ataitia mkononi
mwa mfalme."

13 Mjumbe aliyekuwa amekwenda
kumwita Mikaya akamwambia, "Tazama,
manabii wote kama mtu mmoja wanatabiri
ushindi kwa mfalme. Neno lako na
likubaliane na lao, nawe unene mema
kuhusu mfalme."

14 [b]Lakini Mikaya akasema, "Hakika kama
BWANA aishivyo, nitamwambia kile tu
BWANA atakachoniambia."

15 Alipofika, mfalme akamuuliza,
"Mikaya, je, twende vitani dhidi ya Ramoth-
Gileadi au niache?"

Akamjibu, "Shambulia na ushinde, kwa
kuwa BWANA atawatia mkononi mwa
mfalme."

16 Mfalme akamwambia, "Je, ni mara
ngapi nitakuapisha ili usiniambie kitu
chochote ila kweli tu kwa jina la BWANA?"

17 [c]Ndipo Mikaya akajibu, "Niliona Israeli
wote wametawanyika vilimani kama
kondoo wasio na mchungaji, naye BWANA
akasema, 'Watu hawa hawana bwana.
Mwache kila mmoja aende nyumbani kwa
amani.' "

18 Mfalme wa Israeli akamwambia
Yehoshafati, "Sikukuambia kwamba huwa
hatabiri jambo lolote jema kunihusu, bali
mabaya tu?"

19 [d]Mikaya akaendelea, "Kwa hiyo lisikie
neno la BWANA: Nilimwona BWANA
ameketi juu ya kiti chake cha enzi pamoja
na jeshi lote la mbinguni likiwa limesimama
kumzunguka upande wa kulia na wa
kushoto. 20 Naye BWANA akasema, 'Ni nani
atakayemshawishi Ahabu ili aishambulie
Ramoth-Gileadi na kukiendea kifo chake
huko?'

"Mmoja akapendekeza hili na mwingine
lile. 21 Mwishoni, pepo mchafu akajitokeza,
akasimama mbele za BWANA na kusema,
'Nitamshawishi.'

22 [e]"BWANA akauliza, 'Kwa njia gani?'

"Akasema, 'Nitakwenda na kuwa roho
ya uongo katika vinywa vya manabii wake
wote.'

"BWANA akasema, 'Utafanikiwa katika
kumshawishi. Nenda ukafanye hivyo.'

23 [f]"Kwa hiyo sasa BWANA ameweka roho
ya kudanganya ndani ya vinywa vya hawa
manabii wako wote. BWANA ameamuru
maafa kwa ajili yako."

24 Kisha Sedekia mwana wa Kenaana
akatoka na kumpiga Mikaya kofi usoni.
Akauliza, "Huyo Roho kutoka kwa BWANA
alipita njia gani alipotoka kwangu ili
kusema nawe?"

25 [g]Mikaya akajibu, "Utagundua siku hiyo
utakapokwenda kujificha kwenye chumba
cha ndani."

26 Kisha mfalme wa Israeli akaagiza,
"Mchukueni na mkamrudishe kwa Amoni
mtawala wa mji na kwa Yoashi mwana
wa mfalme. 27 [h]Mkaseme, 'Hivi ndivyo
asemavyo mfalme: Mwekeni mtu huyu

[a]**22:11** Kum 33:17; Zek 1:18-21
[b]**22:14** Hes 22:18
[c]**22:17** Mt 9:36
[d]**22:19** Isa 6:1; Dan 7:9; Ay 1:6
[e]**22:22** Amu 9:23; 2The 2:11
[f]**22:23** Eze 14:9; Kum 31:29
[g]**22:25** 1Fal 20:30
[h]**22:27** 2Nya 16:10; Ebr 11:36

gerezani na asipewe chochote ila mkate
na maji mpaka nitakaporudi salama.' "
28 [a]Mikaya akasema, "Kama utarudi
salama, basi BWANA hajanena kupitia
kwangu." Kisha akaongeza kusema,
"Zingatieni maneno yangu, enyi watu
wote!"

*Ahabu Auawa Ramoth-Gileadi*

**(2 Nyakati 18:28-34)**

29 Basi mfalme wa Israeli na Yehoshafati
mfalme wa Yuda wakaenda Ramoth-
Gileadi. 30 [b]Mfalme wa Israeli akamwambia
Yehoshafati, "Nitaingia vitani nikiwa
nimejibadilisha, lakini wewe uvae majoho
yako ya kifalme." Kwa hiyo mfalme wa
Israeli akajibadilisha na kwenda vitani.
31 [c]Wakati huu, mfalme wa Aramu
alikuwa amewaagiza majemadari thelathini
na wawili wa magari ya vita, "Msipigane
na yeyote, mdogo au mkubwa, isipokuwa
mfalme wa Israeli." 32 Wakati wale
majemadari wa magari ya vita walipomwona
Yehoshafati wakafikiri, "Hakika huyu ndiye
mfalme wa Israeli." Kwa hiyo wakageuka ili
wamshambulie, lakini Yehoshafati akapiga
kelele, 33 wale majemadari wakaona
kwamba hakuwa mfalme wa Israeli, nao
wakaacha kumfuatilia.
34 [d]Lakini mtu fulani akavuta upinde
pasipo lengo na kumpiga mfalme wa Israeli
katikati ya kiungio cha mavazi yake ya
chuma. Mfalme akamwambia mwendesha
gari lake, "Geuza gari na uniondoe mimi
katika mapigano, nimejeruhiwa." 35 Vita
vikaendelea mchana kutwa, naye Mfalme
Ahabu akategemezwa ndani ya gari
kuelekea Waaramu. Damu kutoka kwenye
jeraha lake ikachuruzika ndani ya gari na
jioni yake akafa. 36 Jua lilipokuwa linazama,
mbiu ikaenea katika jeshi lote: "Kila mtu
aende mjini kwake, na kila mtu shambani
kwake!"
37 Basi mfalme akafa na akaletwa Samaria,
nao wakamzika huko. 38 [e]Wakasafisha
lile gari la vita katika bwawa la Samaria
(mahali makahaba walipooga), na mbwa
wakaramba damu yake, sawasawa na neno
la BWANA lilivyokuwa limesema.
39 [f]Kwa matukio mengine ya utawala wa
Ahabu, pamoja na yote aliyoyafanya, jumba
la kifalme alilojenga na kupambwa kwa
pembe za ndovu, nayo miji aliyoijengea
maboma, je, hayakuandikwa katika kitabu
cha kumbukumbu za wafalme wa Israeli?
40 Ahabu akalala pamoja na baba zake.
Naye Ahazia mwanawe akawa mfalme
baada yake.

*Yehoshafati Mfalme Wa Yuda*

**(2 Nyakati 20:31–21:1)**

41 Yehoshafati mwana wa Asa akawa
mfalme wa Yuda katika mwaka wa nne wa
Ahabu mfalme wa Israeli. 42 Yehoshafati
alikuwa na umri wa miaka thelathini na
mitano alipoanza kutawala, naye akatawala
huko Yerusalemu miaka ishirini na mitano.
Jina la mama yake aliitwa Azuba binti
Shilhi. 43 [g]Katika kila jambo alitembea
katika njia za Asa baba yake wala hakwenda
kinyume chake. Alifanya yaliyo mema
machoni pa BWANA. Hata hivyo mahali pa
juu pa kuabudia hapakuondolewa. Watu
waliendelea kutoa kafara na kufukiza
uvumba huko. 44 Yehoshafati pia alikuwa
na amani na mfalme wa Israeli.
45 Kwa habari ya matukio mengine
ya utawala wa Yehoshafati, mafanikio
aliyokuwa nayo na uhodari wake katika
vita, je, hayakuandikwa katika kitabu
cha kumbukumbu za wafalme wa Yuda?
46 [h]Aliondolea mbali katika nchi mahanithi
wa mahali pa kuabudia miungu waliobaki
huko hata baada ya utawala wa baba yake
Asa. 47 [i]Tangu hapo hapakuwepo na mfalme
katika Edomu, naibu ndiye alitawala.
48 [j]Wakati huu Yehoshafati akaunda
merikebu nyingi za biashara[k] ili kwenda

[a]**22:28** Kum 18:22
[b]**22:30** 1Sam 28:8
[c]**22:31** Mwa 10:22; 2Sam 10:19
[d]**22:34** 2Fal 9:24; 2Nya 35:23
[e]**22:38** 1Fal 21:19
[f]**22:39** Za 45:8; Amo 3:15
[g]**22:43** 2Nya 17:3; 1Fal 3:2
[h]**22:46** Kum 23:17
[i]**22:47** 2Fal 3:9; 8:20
[j]**22:48** 1Fal 9:26; Hes 33:35
[k]48 Au: za Tarshishi (ona pia 1Fal 10:22;
2Nya 9:21; 20:36; Isa 2:16; 60:9).

Ofiri kuchukua dhahabu, lakini kamwe
hazikusafiri, kwa maana zilivunjika huko
Esion-Geberi. 49 Wakati ule, Ahazia mwana
wa Ahabu akamwambia Yehoshafati,
“Waache watu wangu wasafiri baharini
pamoja na watu wako,” lakini Yehoshafati
akakataa.

50 Kisha Yehoshafati akalala na baba
zake, akazikwa pamoja nao katika mji wa
Daudi baba yake. Mwanawe Yehoramu
akawa mfalme baada yake.

*Ahazia Mfalme Wa Israeli*

51 Ahazia mwana wa Ahabu akawa
mfalme wa Israeli huko Samaria katika
mwaka wa kumi na saba wa Yehoshafati
mfalme wa Yuda, naye alitawala katika
Israeli kwa miaka miwili. 52 [a]Akafanya
maovu machoni mwa Bwana kwa sababu
alienenda katika njia za baba yake na
mama yake na katika njia za Yeroboamu
mwana wa Nebati, ambaye alisababisha
Israeli itende dhambi. 53 [b]Alimtumikia na
kumwabudu Baali na kumghadhibisha
Bwana, Mungu wa Israeli, kama vile baba
yake alivyokuwa amefanya.

---

[a]**22:52** 1Fal 15:26
[b]**22:53** Amu 2:11; 1Fal 21:25

# 2 WAFALME

*Hukumu Ya Bwana Juu Ya Ahazia*

1 [a]Baada ya kifo cha Mfalme Ahabu, nchi
ya Moabu iliasi dhidi ya Israeli. 2 [b]Basi
Ahazia alikuwa ameanguka huko Samaria
kutoka baraza ya chumba chake cha
juu, akaumia. Hivyo akatuma wajumbe,
akiwaambia, "Nendeni mkaulize kwa Baal-
Zebubu, mungu wa Ekroni, mkaone kama
nitapona kutokana na kuumia huku."
3 [c]Lakini malaika wa Bwana
akamwambia Eliya, Mtishbi, "Panda
ukakutane na wajumbe wa mfalme wa
Samaria, uwaulize, 'Je, ni kwa sababu
hakuna Mungu katika Israeli ndiyo maana
mnakwenda kumuuliza Baal-Zebubu,
mungu wa Ekroni?' 4 [d]Kwa hiyo hili ndilo
asemalo Bwana, 'Hutaondoka kwenye
kitanda unachokilalia. Hakika utakufa!' "
Hivyo Eliya akaenda.
5 Wajumbe waliporudi kwa mfalme,
akawauliza, "Kwa nini mmerudi?"
6 [e]Wakamjibu, "Mtu fulani alikuja
kukutana nasi, naye akatuambia, 'Rudini
kwa mfalme aliyewatuma na mkamwambie,
"Hili ndilo asemalo Bwana: Je, ni kwa
sababu hakuna Mungu katika Israeli ndiyo
maana unawatuma watu kwenda kuuliza
kwa Baal-Zebubu, mungu wa Ekroni?
Kwa hiyo hutaondoka kwenye kitanda
unachokilalia. Hakika utakufa!" ' "
7 Mfalme akawauliza, "Alikuwa mtu
wa namna gani ambaye mlikutana naye,
akawaambia hili?"
8 [f]Wakamjibu, "Alikuwa mtu aliyekuwa
na vazi la manyoya na mkanda wa ngozi
kiunoni mwake."
Mfalme akasema, "Huyo alikuwa ni Eliya,
Mtishbi."
9 [g]Ndipo mfalme akamtuma mkuu mmoja
wa kikosi pamoja na kikosi chake cha askari
hamsini kwa nabii Eliya. Yule mkuu wa
kikosi akamwendea Eliya, aliyekuwa
ameketi juu ya kilima, na kumwambia,
"Mtu wa Mungu, mfalme anasema, 'Shuka
chini!' "
10 [h]Eliya akamjibu yule mkuu wa kikosi,
"Ikiwa mimi ni mtu wa Mungu, moto na
ushuke kutoka mbinguni ukuteketeze
wewe na watu wako hamsini!" Ndipo moto
ukashuka kutoka mbinguni na kuwateketeza
yule mkuu wa kikosi pamoja na watu wake.
11 [i]Aliposikia hili, mfalme akatuma
kwa Eliya mkuu wa kikosi mwingine na
askari wake hamsini. Yule mkuu wa kikosi
akamwambia Eliya, "Mtu wa Mungu, hili
ndilo asemalo mfalme, 'Shuka chini mara
moja!' "
12 Eliya akajibu, "Ikiwa mimi ni mtu wa
Mungu, moto na ushuke kutoka mbinguni
ukuteketeze wewe na watu wako hamsini!"
Ndipo moto wa Mungu ukashuka kutoka
mbinguni, ukamteketeza yeye na watu
wake hamsini.
13 [j]Hivyo mfalme akatuma mkuu wa
kikosi wa tatu na watu wake hamsini. Huyu
mkuu wa kikosi wa tatu akapanda na kupiga
magoti mbele ya Eliya, akiomba, "Mtu wa
Mungu, tafadhali niachie uhai wangu na
uhai wa hawa watu hamsini, watumishi
wako! 14 Tazama, moto umeshuka kutoka
mbinguni na kuwateketeza wale wakuu wa
vikosi viwili vya kwanza pamoja na watu
wao. Lakini sasa niachie uhai wangu!"
15 [k]Malaika wa Bwana akamwambia
Eliya, "Shuka pamoja naye, usimwogope."

---

[a]**1:1** Mwa 19:37; 2Sam 8:2; 2Fal 3:5
[b]**1:2** Amu 18:5; 2Fal 1:16; 8:7-10; Mt 10:25; Isa 14:29; Mk 3:22; 1Sam 5:10
[c]**1:3** Mwa 16:7; 1Sam 28:8; Isa 8:19; Yer 2:10-13; Yon 2:8
[d]**1:4** 2Fal 1:6, 16; Za 41:8; Rum 6:23; Mhu 8:13; Mit 11:19; Isa 3:11; Yak 1:15
[e]**1:6** 2Fal 1:2; Mit 14:32
[f]**1:8** Isa 3:3; Zek 13:4; Mt 3:4
[g]**1:9** Kut 18:25; 2Fal 6:14; Za 105:15; Amo 7:12; Mt 27:29
[h]**1:10** Hes 11:1; 1Fal 18:38; Lk 9:54; Ufu 11:5
[i]**1:11** Isa 26:11
[j]**1:13** 1Sam 26:21; Za 72:14; Mit 22:27; Mhu 9:3; Yer 5:3
[k]**1:15** 2Fal 1:3; Isa 57:11-12; Yer 1:17; Eze 2:6

Hivyo Eliya akainuka na kushuka pamoja
naye kwa mfalme.
16 Akamwambia mfalme, “Hili ndilo
asemalo BWANA: Je, ni kwa sababu hakuna
Mungu katika Israeli wa kumuuliza habari,
ndiyo maana ukatuma wajumbe kuuliza
Baal-Zebubu, mungu wa Ekroni? Kwa
sababu umefanya hili, kamwe hutaondoka
kwenye kitanda unachokilalia. Hakika
utakufa!” 17 [a]Hivyo akafa, sawasawa na
lile neno la BWANA ambalo Eliya alikuwa
amesema.
Kwa kuwa Ahazia hakuwa na mwana,
Yoramu[b] akawa mfalme baada yake katika
mwaka wa pili wa Yehoramu mwana wa
Yehoshafati mfalme wa Yuda. 18 Kwa
matukio mengine ya utawala wa Ahazia
na yale aliyoyafanya, je, hayakuandikwa
katika kitabu cha kumbukumbu za wafalme
wa Israeli?

*Eliya Achukuliwa Mbinguni*

2 [c]Wakati BWANA alipokuwa karibu
kumchukua Eliya mbinguni kwa
upepo wa kisulisuli, Eliya na Elisha
walikuwa njiani wakitoka Gilgali. 2 [d]Eliya
akamwambia Elisha, “Kaa hapa. BWANA
amenituma Betheli.”
Lakini Elisha akasema, “Kwa hakika,
kama BWANA aishivyo na wewe uishivyo,
sitakuacha.” Kwa hiyo wakaenda Betheli
pamoja.
3 [e]Wana wa manabii waliokuwako huko
Betheli wakamjia Elisha na kumuuliza, “Je,
unajua ya kwamba BWANA atakuondolea
bwana wako leo?”
Elisha akawajibu, “Ndiyo, najua, lakini
msizungumze juu ya jambo hilo.”
4 [f]Kisha Eliya akamwambia, “Baki hapa,
Elisha. BWANA amenituma Yeriko.”
Naye akajibu, “Kwa hakika kama BWANA
aishivyo na wewe uishivyo, sitakuacha.”
Hivyo wakaenda Yeriko.

5 [g]Wana wa manabii waliokuwako
huko Yeriko wakamwendea Elisha na
kumuuliza, “Je, unajua ya kwamba BWANA
atakuondolea bwana wako leo?”
Akawajibu, “Ndiyo, najua, lakini
msizungumze juu ya jambo hilo.”
6 [h]Kisha Eliya akamwambia, “Kaa hapa.
BWANA amenituma kwenda Yordani.”
Naye akamjibu, “Kwa hakika kama BWANA
aishivyo na wewe uishivyo, sitakuacha.”
Hivyo wote wawili wakaendelea pamoja.
7 Wana hamsini wa manabii wakaenda
na kusimama kwa mbali, kuelekea
mahali ambapo Eliya na Elisha walikuwa
wamesimama kando ya Mto Yordani.
8 [i]Eliya akachukua vazi lake, akalisokota
na kupiga nalo maji. Maji yakagawanyika
upande wa kuume na upande wa kushoto,
nao wawili wakavuka pakavu.
9 [j]Walipokwisha kuvuka, Eliya
akamwambia Elisha, “Niambie, nikufanyie
nini kabla sijaondolewa kutoka kwako?”
Elisha akajibu, “Naomba nirithi sehemu
maradufu ya roho yako.”
10 Eliya akasema, “Umeomba jambo
gumu. Lakini kama utaniona wakati
ninapoondolewa kutoka kwako litakuwa
lako. La sivyo, hautalipata.”
11 [k]Walipokuwa wakitembea pamoja na
kuzungumza, ghafula gari la moto na farasi
wa moto vilitokea na kuwatenganisha wao
wawili, naye Eliya akapanda mbinguni
katika upepo wa kisulisuli. 12 [l]Elisha aliona
hili, naye akapaza sauti, “Baba yangu! Baba
yangu! Magari ya Israeli na wapanda farasi
wake!” Naye Elisha hakumwona tena.
Kisha akazishika nguo zake mwenyewe na
kuzirarua.
13 Akaliokota lile vazi lililoanguka
kutoka kwa Eliya, kisha akarudi na
kusimama ukingoni mwa Yordani. 14 [m]Ndipo
akalichukua lile vazi ambalo lilikuwa
limeanguka kutoka kwa Eliya, naye

[a]**1:17** 2Fal 8:15-16; Yer 20:6; 28:17
[b]17 Yoramu ni namna nyingine ya kutaja jina Yehoramu.
[c]**2:1** Mwa 5:24; 1Fal 19:16
[d]**2:2** Rut 1:16
[e]**2:3** 1Sam 10:5
[f]**2:4** Yos 3:16
[g]**2:5** 2Fal 2:3
[h]**2:6** Yos 3:15
[i]**2:8** Kut 14:21
[j]**2:9** Kum 21:17; Hes 11:17
[k]**2:11** 2Fal 6:17; Za 104:3, 4
[l]**2:12** 2Fal 13:14; Mwa 37:29
[m]**2:14** 1Fal 19:19

akayapiga yale maji nalo. Akauliza, "Yuko
wapi sasa BWANA, Mungu wa Eliya?" Elisha
alipoyapiga maji, yakagawanyika kulia na
kushoto, naye akavuka.
15 [a]Wale wana wa manabii kutoka Yeriko
waliokuwa wakitazama wakasema, "Roho
wa Eliya inamkalia Elisha." Nao wakaenda
kumlaki na kusujudu hadi nchi mbele yake.
16 [b]Wakasema, "Tazama, sisi watumishi
wako tunao watu hamsini wenye uwezo.
Waruhusu waende kumtafuta bwana wako.
Labda Roho wa BWANA amemtwaa na
kumweka katika mlima fulani au bonde
fulani."
Elisha akajibu, "Hapana, msiwatume."
17 [c]Lakini wakasisitiza, mpaka akaona
aibu kuwakatalia. Hivyo akasema,
"Watumeni." Nao wakawatuma watu
hamsini, wakamtafuta kwa siku tatu, lakini
hawakumpata. 18 Walipomrudia Elisha,
ambaye alikuwa akingojea huko Yeriko,
akawaambia, "Je, sikuwaambia msiende?"

*Kuponywa Kwa Maji*

19 Watu wa mji wakamwambia Elisha,
"Tazama, bwana wetu, mahali mji huu
ulipojengwa ni pazuri, kama bwana wangu
aonavyo, lakini maji yake ni mabaya, na
nchi haizai."
20 Akasema, "Nileteeni bakuli mpya,
mweke chumvi ndani yake." Kwa hiyo
wakamletea.
21 [d]Kisha akaenda kwenye chemchemi na
kuitupa ile chumvi ndani yake, akisema,
"Hili ndilo asemalo BWANA: 'Nimeyaponya
maji haya. Kamwe hayatasababisha mauti
tena wala kutozaa.' " 22 [e]Nayo yale maji
yakaponywa mpaka leo, sawasawa na neno
la Elisha alilokuwa amesema.

*Elisha Anafanyiwa Mzaha*

23 [f]Kutoka huko Elisha akakwea kwenda
Betheli. Ikawa alipokuwa akitembea
barabarani, baadhi ya vijana wakatoka
mjini na kumfanyia mzaha. Wakasema,
"Paa, wewe mwenye upaa! Paa, wewe
mwenye upaa!" 24 [g]Akageuka, akawatazama
na kuwalaani kwa Jina la BWANA. Kisha
dubu wawili wa kike wakatokea mwituni
na kuwararua vijana arobaini na wawili
miongoni mwao. 25 Naye akaondoka huko,
akaenda Mlima Karmeli, na kutoka huko
akarudi Samaria.

*Moabu Wanaasi*

3 [h]Yehoramu[i] mwana wa Ahabu akawa
mfalme wa Israeli katika Samaria
mwaka wa kumi na nane wa utawala
wa Yehoshafati mfalme wa Yuda, naye
akatawala kwa miaka kumi na miwili.
2 [j]Akafanya maovu machoni pa BWANA,
lakini sio kama baba yake na mama yake
walivyokuwa wamefanya. Akaondoa
nguzo ya ibada ya Baali ambayo baba
yake alikuwa ameitengeneza. 3 [k]Hata hivyo
akashikamana na dhambi za Yeroboamu
mwana wa Nebati, ambazo alisababisha
Israeli kuzitenda, wala hakuziacha.
4 [l]Basi Mesha mfalme wa Moabu akafuga
kondoo, naye akawa ampatie mfalme wa
Israeli wana-kondoo 100,000 pamoja na
sufu ya kondoo dume 100,000. 5 [m]Lakini
baada ya Ahabu kufa, mfalme wa Moabu
aliasi dhidi ya mfalme wa Israeli. 6 Kwa hiyo
wakati ule Mfalme Yehoramu akaondoka
kutoka Samaria na kukusanya Israeli yote
tayari kwenda vitani. 7 [n]Akapeleka pia
ujumbe ufuatao kwa Yehoshafati mfalme
wa Yuda: "Mfalme wa Moabu ameasi
dhidi yangu. Je, utakwenda pamoja nami
kupigana dhidi ya Moabu?"
Akajibu, "Nitakwenda pamoja nawe.
Mimi ni kama wewe, watu wangu ni kama
watu wako, farasi wangu ni kama farasi
wako."

---

[a]**2:15** 1Sam 10:5; Hes 11:17
[b]**2:16** 1Fal 18:12; Mdo 8:39
[c]**2:17** Amu 3:25
[d]**2:21** Kut 15:25; 2Fal 4:41; 6:6
[e]**2:22** Kut 15:22
[f]**2:23** 2Nya 30:10; Za 31:18
[g]**2:24** Mwa 4:11; Kum 18:19
[h]**3:1** 2Fal 1:17
[i]1 Yehoramu wakati mwingine limetajwa kama Yoramu.
[j]**3:2** 1Fal 16:30; Kut 23:24
[k]**3:3** 1Fal 12:30
[l]**3:4** Mwa 19:37; Isa 16:1
[m]**3:5** 2Fal 1:1
[n]**3:7** 1Fal 22:4

8 Akauliza, “Je, tutashambulia kupitia
njia gani?”
Akajibu, “Kupitia Jangwa la Edomu.”
9 [a]Hivyo mfalme wa Israeli akaondoka
akiwa pamoja na mfalme wa Yuda na
mfalme wa Edomu. Baada ya kuzunguka
kwa siku saba, jeshi likawa limeishiwa maji
kwa matumizi yao na kwa ajili ya wanyama
waliokuwa nao.
10 Mfalme wa Israeli akamaka, “Nini! Je,
Bwana ametuita sisi wafalme watatu ili tu
kututia mikononi mwa Moabu?”
11 [b]Lakini Yehoshafati akauliza, “Je,
hayuko nabii wa Bwana hapa, ili tuweze
kumuuliza Bwana kupitia kwake?”
Afisa mmoja wa mfalme wa Israeli
akajibu, “Elisha mwana wa Shafati yuko
hapa. Ndiye alikuwa akimimina maji juu
ya mikono ya Eliya.”
12 [c]Yehoshafati akasema, “Neno la Bwana
liko pamoja naye.” Kwa hiyo mfalme wa
Israeli na Yehoshafati pamoja na mfalme
wa Edomu wakamwendea.
13 Elisha akamwambia mfalme wa Israeli,
“Nina nini mimi nawe? Nenda kwa manabii
wa baba yako na manabii wa mama yako.”
Mfalme wa Israeli akajibu, “La hasha,
kwa sababu ni Bwana ambaye ametuita
pamoja sisi wafalme watatu ili atutie
mikononi mwa Moabu.”
14 Elisha akasema, “Hakika, kama
Bwana Mwenye Nguvu Zote aishivyo
ambaye ninamtumikia, kama si
kuheshimu Yehoshafati mfalme wa Yuda,
nisingekutazama wala hata kukutupia jicho.
15 [d]Lakini sasa, nileteeni mpiga kinubi.”
Mpiga kinubi alipokuwa akipiga, mkono
wa Bwana ukaja juu ya Elisha, 16 naye
akasema, “Hivi ndivyo asemavyo Bwana,
‘Chimbeni bonde hili lijae mahandaki.’
17 Kwa kuwa hivi ndivyo asemavyo Bwana:
Hamtaona upepo wala mvua, lakini
bonde hili litajaa maji, nanyi pamoja na
ng’ombe wenu na wanyama wenu wengine
mtakunywa. 18 [e]Hili ni jambo rahisi machoni
pa Bwana. Pia ataitia Moabu mikononi
mwenu. 19 Mtaushinda kila mji wenye
ngome na kila mji mkubwa. Mtakata kila
mti ulio mzuri, mtaziba chemchemi zote,
na kuharibu kila shamba zuri kwa mawe.”
20 [f]Kesho yake asubuhi, karibu na wakati
wa kutoa dhabihu ya asubuhi, tazama, maji
yakawa yanatiririka kutoka upande wa
Edomu! Nayo nchi ikajaa maji.
21 Basi Wamoabu wote walikuwa
wamesikia kuwa wale wafalme wamekuja
kupigana dhidi yao. Hivyo kila mtu, kijana
na mzee, ambaye angeweza kushika
silaha akaitwa na kuwekwa mpakani.
22 Walipoamka asubuhi na mapema, jua
likawa linamulika juu ya maji. Wamoabu
waliokuwa upande wa pili wakaona maji
ni mekundu, kama damu. 23 Wamoabu
wakasema, “Ile ni damu! Lazima hao
wafalme wamepigana na kuchinjana wao
kwa wao. Sasa Moabu, twendeni tukateke
nyara!”
24 Lakini Wamoabu walipofika kwenye
kambi ya Israeli, Waisraeli wakainuka
na kuwapiga mpaka wakakimbia. Nao
Waisraeli wakaivamia nchi na kuwachinja
Wamoabu. 25 [g]Wakaiharibu miji, kila mtu
akatupa jiwe juu ya kila shamba zuri mpaka
likafunikwa. Wakaziba chemchemi zote na
kukata kila mti mzuri. Kir-Haresethi peke
yake ndio uliobaki na mawe yake yakiwa
mahali pake. Lakini hata hivyo watu
waliokuwa na makombeo wakauzunguka
na kuushambulia vilevile.
26 Mfalme wa Moabu alipoona kuwa vita
vimekuwa vikali dhidi yake, akachukua
watu 700 wenye panga ili kuingia kwa
mfalme wa Edomu, lakini wakashindwa.
27 [h]Ndipo akamchukua mwanawe mzaliwa
wake wa kwanza, ambaye angekuwa
mfalme baada yake, akamtoa kama dhabihu
ya kuteketezwa juu ya ukuta wa mji.
Ghadhabu ikawa kubwa dhidi ya Israeli;
wakajiondoa kwake na kurudi katika nchi
yao wenyewe.

---

[a]**3:9** 1Fal 22:47
[b]**3:11** Mwa 25:22; 1Fal 19:16
[c]**3:12** Hes 11:17
[d]**3:15** 1Sam 10:5; Eze 1:3
[e]**3:18** Mwa 18:14; Yer 32:17, 27; Mk 10:27
[f]**3:20** Kut 29:41
[g]**3:25** Isa 16:7; Yer 48:31, 36
[h]**3:27** Za 106:38; Mik 6:7

*Mafuta Ya Mjane*

4 [a]Mke wa mmoja wa wana wa manabii
akamlilia Elisha, akamwambia,
“Mtumishi wako, mume wangu, amekufa,
nawe unajua alikuwa anamcha BWANA.
Lakini sasa yule anayemdai anakuja
kuchukua wanangu wawili kama watumwa
wake.”
2 [b]Elisha akamjibu, “Nitawezaje
kukusaidia? Niambie, una nini ndani ya
nyumba yako?”
Akasema, “Mtumishi wako hana kitu
chochote kabisa, isipokuwa mafuta kidogo.”
3 Elisha akasema, “Zunguka kwa majirani
zako wote ukaombe vyombo vitupu.
Usiombe vichache. 4 Kisha ingia ndani na
ujifungie mlango, wewe na wanao. Mimina
mafuta kwenye vyombo vyote, na kila
kimoja kinapojaa, kiweke kando.”
5 Yule mjane akaondoka na kujifungia
ndani, yeye na wanawe. Wao wakamletea
vyombo, naye akaendelea kumimina
mafuta. 6 Vyombo vyote vilipojaa,
akamwambia mwanawe, “Niletee chombo
kingine.”
Lakini mwanawe akajibu, “Hakuna
chombo kingine kilichobaki.” Basi mafuta
yakakoma kutiririka.
7 [c]Yule mwanamke akaenda akamwambia
yule mtu wa Mungu, naye mtu wa Mungu
akasema, “Nenda ukayauze hayo mafuta
ulipe madeni yako. Wewe na wanao
mnaweza kuishi kwa kile kinachosalia.”

*Mwana Wa Mshunami Afufuliwa*

8 [d]Siku moja Elisha akaenda Shunemu.
Huko kulikuwa na mwanamke mmoja
mwenye cheo, ambaye alimsisitiza Elisha
aje kula chakula. Kwa hiyo kila mara alipitia
pale, akaingia humo ili ale. 9 Akamwambia
mumewe, “Ninajua kwamba huyu mtu
ambaye anakuja kwetu mara kwa mara ni
mtu mtakatifu wa Mungu. 10 [e]Tutengeneze
chumba kidogo juu darini na tuweke ndani
yake kitanda na meza, kiti na taa kwa ajili
yake. Kisha anaweza kukaa humo kila mara
akija kwetu.”
11 Siku moja Elisha alipofika, akapanda
chumbani kwake na kulala humo.
12 [f]Akamwambia mtumishi wake Gehazi,
“Mwite huyo Mshunami.” Hivyo akamwita,
naye akaja akasimama mbele yake. 13 Elisha
akamwambia mtumishi wake, “Mwambie
huyu mwanamke, ‘Umetaabika sana kwa
ajili yetu. Sasa utendewe nini? Je, tunaweza
kuzungumza na mfalme au jemadari wa
jeshi kwa niaba yako?’ ”
Akajibu, “Mimi ninaishi kwangu
miongoni mwa watu wangu.”
14 Elisha akamwambia mtumishi wake,
“Je, ni nini kinachoweza kufanyika kwa
ajili yake?”
Gehazi akasema, “Hakika, hana mwana,
na mume wake ni mzee.”
15 Ndipo Elisha akasema, “Mwite huyo
mwanamke.” Kwa hiyo akamwita, naye
akaja akasimama mlangoni. 16 [g]Elisha
akamwambia, “Mwaka ujao, wakati kama
huu utabeba mwana mikononi mwako.”
Yule mama akapinga, akasema, “La
hasha, bwana wangu, usimpotoshe
mtumishi wako, ee mtu wa Mungu!”
17 Lakini yule mwanamke akapata
mimba, na mwaka uliofuata wakati kama
ule ule akamzaa mwana, kama vile Elisha
alivyokuwa amemwambia.
18 [h]Mtoto akakua, naye siku moja
akamwendea baba yake, ambaye alikuwa
pamoja na wavunaji. 19 Akamwambia baba
yake, “Kichwa changu! Kichwa changu!”
Baba yake akamwambia mtumishi,
“Mchukue umpeleke kwa mama yake.”
20 Baada ya mtumishi kumbeba na
kumpeleka kwa mama yake, mtoto akaketi
mapajani mwa mama yake mpaka adhuhuri,
kisha akafa. 21 [i]Mama akampandisha na
kumlaza juu ya kitanda cha yule mtu wa
Mungu, kisha akafunga mlango, akatoka
nje.
22 Akamwita mume wake na kusema,
“Tafadhali mtume mmoja miongoni mwa

[a]**4:1** Law 25:39-43; Neh 5:3-5
[b]**4:2** 1Fal 17:12
[c]**4:7** 1Fal 12:22
[d]**4:8** Yos 19:18
[e]**4:10** Mt 10:41; Rum 12:13
[f]**4:12** 2Fal 8:1
[g]**4:16** Mwa 18:10
[h]**4:18** Rut 2:3
[i]**4:21** 2Fal 4:32

mtumishi pamoja na punda ili niweze
kwenda kwa mtu wa Mungu haraka na
kurudi."
23 [a]Mume wake akamuuliza, "Kwa nini
uende kwake leo? Leo si mwandamo wa
mwezi, wala si Sabato."
Mwanamke akasema, "Yote ni sawa."
24 Akatandika punda na kumwambia
mtumishi wake, "Mwongoze huyo punda.
Usinipunguzie mwendo mpaka nikuambie."
25 [b]Kwa hiyo akaenda na kumfikia huyo mtu
wa Mungu katika Mlima Karmeli.
Alipomwona kwa mbali, huyo mtu
wa Mungu akamwambia mtumishi wake
Gehazi, "Tazama, yule Mshunami! 26 Kimbia
ukamlaki, umuulize, 'Je, wewe hujambo?
Mume wako hajambo? Mtoto wako ni
mzima?' "
Akasema, "Kila kitu ni sawasawa."
27 [c]Alipomfikia huyo mtu wa Mungu pale
mlimani, akashika miguu yake. Gehazi akaja
ili amwondoe, lakini yule mtu wa Mungu
akasema, "Mwache! Yuko katika uchungu
mkubwa, lakini BWANA amenificha jambo
hili na hajaniambia kwa nini."
28 Yule mwanamke akasema, "Je,
bwana wangu, mimi nilikuomba mwana?
Je, sikukuambia, 'Usiamshe matumaini
yangu'?"
29 [d]Elisha akamwambia Gehazi, "Jikaze
viuno, chukua fimbo yangu mkononi
mwako na ukimbie. Ikiwa utakutana na
mtu yeyote, usimsalimie, na mtu yeyote
akikusalimu, usimjibu. Ilaze fimbo yangu
juu ya uso wa mtoto."
30 Lakini mama mtoto akasema, "Hakika
kama BWANA aishivyo na wewe uishivyo,
sitakuacha." Kwa hiyo Elisha akainuka,
akafuatana naye.
31 Gehazi akatangulia mbele na kuilaza
fimbo juu ya uso wa mtoto, lakini hapakuwa
na sauti wala itikio. Hivyo Gehazi akarudi
kukutana na Elisha, na kumwambia, "Mtoto
hajaamka."
32 Elisha alipofika kwenye ile nyumba,
mtoto alikuwa amelala juu ya kitanda
chake angali amekufa. 33 [e]Akaingia ndani,
akajifungia yeye na yule mtoto, akamwomba
BWANA. 34 [f]Kisha akapanda kitandani,
akalala juu ya yule mtoto, mdomo wake
juu ya mdomo wa mtoto, macho yake juu
ya macho ya mtoto, mikono yake juu ya
mikono ya mtoto. Naye alipojinyoosha
juu yake, mwili wa mtoto ukapata joto.
35 [g]Elisha akajiondoa juu yake na kuanza
kutembeatembea ndani ya chumba, kisha
akarudi tena kitandani na kujinyoosha tena
juu ya mtoto mara nyingine. Mtoto akapiga
chafya mara saba, akafungua macho yake.
36 [h]Elisha akamwita Gehazi na
kumwambia, "Mwite huyo Mshunami."
Naye akafanya hivyo. Yule Mshunami
alipokuja, Elisha akasema, "Mchukue
mwanao." 37 Akaingia ndani, akaanguka
miguuni pa Elisha na kusujudu hadi nchi.
Kisha akamchukua mwanawe na kutoka
nje.

### *Mauti Ndani Ya Chungu*

38 [i]Elisha akarudi Gilgali, nako huko
kulikuwa na njaa katika eneo lile. Wakati
wana wa kundi la manabii walipokuwa
wanakutana naye, akamwambia mtumishi
wake, "Teleka chungu kikubwa jikoni
uwapikie manabii."
39 Mmoja wao akatoka kwenda
mashambani kuchuma mboga na akapata
mtango mwitu. Akachuma matango na
kujaza nguo yake aliyoikunja ili kubebea.
Aliporudi, akayakatakata na kuyatumbukiza
ndani ya chungu, ingawa hakuna aliyejua
ni nini. 40 Mchuzi ukagawiwa watu, lakini
walipoanza kula, wakalia, "Ee mtu wa
Mungu, kuna mauti ndani ya chungu." Nao
hawakuweza kula.
41 [j]Elisha akasema, "Leteni unga."
Akauweka ndani ya chungu na kusema,
"Wagawie watu ili wale." Wala hapakuwa
na kitu chochote chenye madhara ndani
ya chungu.

---

[a]**4:23** Hes 10:10; 1Nya 23:31
[b]**4:25** 1Fal 18:20
[c]**4:27** 1Sam 1:15
[d]**4:29** 1Fal 18:46; Kut 4:2
[e]**4:33** 1Fal 17:20; Mt 6:6
[f]**4:34** 1Fal 17:21; Mdo 20:10
[g]**4:35** Yos 6:15; 2Fal 8:5
[h]**4:36** Ebr 11:35
[i]**4:38** 2Fal 2:1; 8:1
[j]**4:41** Kut 15:25; 2Fal 2:21

*Watu Mia Wanalishwa*

42 [a]Akaja mtu kutoka Baal-Shalisha,
akimletea mtu wa Mungu mikate ishirini
ya shayiri iliyookwa kutokana na nafaka
ya kwanza, pamoja na masuke ya nafaka
mpya. Elisha akasema, "Wape watu ili
wale."
43 [b]Mtumishi wake akamuuliza,
"Nitawezaje kuandaa hii mbele ya watu
mia?"

Lakini Elisha akajibu, "Wape watu ili
wale. Kwa maana hivi ndivyo asemavyo
BWANA: 'Watakula na kusaza.' " 44 Basi
akaiandaa mbele yao ile mikate, wakala
na baadhi yake wakasaza, sawasawa na
neno la BWANA.

*Naamani Aponywa Ukoma*

5 [c]Wakati huu, Naamani alikuwa jemadari
wa jeshi la mfalme wa Aramu. Alikuwa
mtu mkuu mbele ya bwana wake na
aliyeheshimiwa sana, kwa sababu kupitia
kwake, BWANA alikuwa amewapa Aramu
ushindi. Alikuwa askari shujaa, lakini
alikuwa na ukoma.[d]
2 [e]Siku hizo vikosi kutoka Aramu vilikuwa
vimekwenda na vikawa vimemteka
msichana kutoka Israeli, naye akamtumikia
mkewe Naamani. 3 [f]Akamwambia bibi yake,
"Kama bwana wangu angelimwona nabii
aliyeko Samaria! Angemponya ukoma
wake."
4 Naamani akaenda kwa bwana wake
na kumwambia alichosema yule msichana
kutoka Israeli. 5 [g]Mfalme wa Aramu[h]
akamjibu, "Hakika, nenda. Nitatuma barua
kwa mfalme wa Israeli." Kwa hiyo Naamani
akaondoka, akiwa amechukua talanta kumi[i]
za fedha, shekeli 6,000 za dhahabu,[j] na
mivao kumi ya mavazi. 6 Barua aliyopelekea
mfalme wa Israeli iliandikwa hivi: "Pamoja
na barua hii ninamtuma mtumishi wangu,
Naamani, kwako ili uweze kumponya
ukoma wake."
7 [k]Mara mfalme wa Israeli alipomaliza
kuisoma ile barua, akararua mavazi yake
na kusema, "Je, mimi ni Mungu? Je, mimi
naweza kuua na kufufua tena? Kwa nini
huyu mtu anamtuma mtu ili mimi nipate
kumponya ukoma wake? Tazama jinsi
anavyotafuta kuanzisha ugomvi nami!"
8 [l]Elisha mtu wa Mungu aliposikia
kwamba mfalme wa Israeli alikuwa
amerarua mavazi yake, akamtumia ujumbe
huu: "Kwa nini umerarua mavazi yako?
Mwamuru mtu huyo aje kwangu, naye
atajua ya kuwa yuko nabii katika Israeli."
9 Kwa hiyo Naamani akaenda, akiwa na
farasi zake na magari yake, na kusimama
mlangoni mwa nyumba ya Elisha. 10 [m]Elisha
akamtuma mjumbe kumwambia, "Nenda
uoge katika Yordani mara saba, na nyama
ya mwili wako itapona, nawe utatakasika."
11 [n]Lakini Naamani akaondoka akiwa
amekasirika, akasema, "Hakika nilidhani
kwamba angetoka nje, asimame na kuliitia
jina la BWANA Mungu wake, na kuweka
mkono wake juu ya mahali pagonjwa,
aniponye ukoma wangu. 12 [o]Je, Abana
na Farpari, mito ya Dameski, si bora
zaidi kuliko mito yoyote ya Israeli? Je,
nisingeweza kuoga ndani ya hiyo mito na
kutakasika?" Basi akageuka na kuondoka
kwa hasira kuu.
13 [p]Watumishi wa Naamani wakamwendea
na kumwambia, "Baba yangu, kama huyo
nabii angekuambia kufanya jambo lililo
kubwa, je, usingelifanya? Je, si zaidi sana
basi, anapokuambia, 'Oga na utakasike!' "

---

[a]**4:42** 1Sam 9:4; Mt 14:17
[b]**4:43** Lk 9:13; Yn 6:12
[c]**5:1** Mwa 10:22; Lk 4:27
[d]1 *Ukoma* ni neno lililotumika kwa Kiebrania kueleza magonjwa mbalimbali ya ngozi ambayo si lazima yawe ni ukoma halisi.
[e]**5:2** 2Fal 6:23
[f]**5:3** Mwa 20:7
[g]**5:5** Mwa 24:53; 1Sam 9:7
[h]5 Yaani mfalme wa Shamu.
[i]5 Talanta 10 za fedha ni sawa na kilo 340.
[j]5 Shekeli 6,000 za dhahabu ni sawa na kilo 70.
[k]**5:7** Mwa 30:2; Kum 32:39; 1Fal 20:7
[l]**5:8** 1Fal 22:7
[m]**5:10** Yn 9:7; Law 14:7
[n]**5:11** Kut 7:19
[o]**5:12** Mit 14:17, 29
[p]**5:13** 2Fal 6:21

14 [a]Hivyo akashuka na kujizamisha ndani
ya Yordani mara saba, kama vile huyo
mtu wa Mungu alivyokuwa amemwambia,
nayo nyama ya mwili wake ikapona na
kutakasika kama ya mwili wa mvulana
mdogo.
15 [b]Kisha Naamani na wahudumu wake
wote wakarudi kwa yule mtu wa Mungu.
Akasimama mbele yake na kusema, "Sasa
najua kwamba hakuna Mungu katika
ulimwengu wote isipokuwa katika Israeli.
Tafadhali sasa upokee zawadi kutoka kwa
mtumishi wako."
16 [c]Nabii akajibu, "Hakika kama BWANA
aishivyo, ambaye ninamtumikia, sitapokea
kitu hata kimoja." Ingawa Naamani alimsihi
sana, yeye alikataa.
17 [d]Naamani akasema, "Ikiwa hutapokea,
tafadhali mtumishi wako na apewe udongo
kiasi cha mzigo wa kuweza kubebwa na
punda wawili, kwa sababu mtumishi wako
hatatoa tena sadaka ya kuteketezwa na
dhabihu kwa mungu mwingine isipokuwa
BWANA. 18 [e]Lakini BWANA na amsamehe
mtumishi wake kwa kitu hiki kimoja:
Wakati bwana wangu atakapoingia kwenye
hekalu la Rimoni ili kusujudu, naye
akiwa anauegemea mkono wangu, nami
nikasujudu huko pia, wakati nitakaposujudu
ndani ya hekalu la Rimoni, BWANA na
amsamehe mtumishi wako kwa ajili ya
jambo hili."
19 [f]Elisha akamwambia, "Nenda kwa
amani."
Baada ya Naamani kusafiri umbali fulani,
20 [g]Gehazi, mtumishi wa Elisha mtu wa
Mungu, akajiambia mwenyewe, "Bwana
wangu amemwachia kirahisi sana Naamani,
huyu Mwaramu, kwa kutokupokea kutoka
kwake vile alivyovileta. Hakika kama
BWANA aishivyo, nitamkimbilia na kupata
kitu kutoka kwake."
21 Hivyo Gehazi akaharakisha kumfuatilia
Naamani. Naamani alipomwona akikimbia
kumwelekea, akashuka chini kutoka kwenye
gari lake na kwenda kumlaki. Akauliza, "Je,
mambo yote ni sawa?"
22 [h]Gehazi akajibu, "Mambo yote ni sawa.
Bwana wangu amenituma nikuambie,
'Vijana wawili kutoka kwa wana wa
manabii wamenijia kutoka nchi ya vilima
ya Efraimu. Tafadhali wape talanta ya
fedha[i] na mivao miwili ya mavazi.' "
23 Naamani akasema, "Hakika, chukua
talanta mbili za fedha." Akamsihi Gehazi
azipokee, kisha akafunga talanta mbili za
fedha katika mifuko miwili pamoja na mivao
miwili ya mavazi. Akawapa watumishi
wake wawili mizigo hiyo, nao wakaibeba
wakitangulia mbele ya Gehazi. 24 Gehazi
alipofika kwenye kilima, akavichukua
vile vitu kutoka kwa wale watumishi na
kuvificha ndani ya nyumba. Akawaaga wale
watu, nao wakaondoka. 25 Kisha akaingia
ndani na kusimama mbele ya Elisha bwana
wake.
Elisha akamuuliza, "Gehazi, ulikuwa
wapi?"
Gehazi akajibu, "Mtumishi wako
hakwenda popote."
26 [j]Lakini Elisha akamwambia, "Je, roho
yangu haikuwa pamoja nawe wakati yule
mtu aliposhuka kutoka kwenye gari lake
ili kukulaki? Je, huu ni wakati wa kupokea
fedha au kupokea nguo, mashamba
ya mizeituni, mashamba ya mizabibu,
makundi ya kondoo na mbuzi, makundi
ya ng'ombe, au watumishi wa kiume na wa
kike? 27 [k]Ukoma wa Naamani utakushika
wewe na wazao wako milele." Kisha Gehazi
akaondoka mbele ya Elisha, mwenye
ukoma, mweupe kama theluji.

*Shoka Laelea*

6 [l]Wana wa manabii wakamwambia Elisha,
"Tazama, mahali hapa tunapokutana
nawe ni padogo sana kwetu. 2 Twendeni
Yordani, mahali ambapo kila mmoja wetu

[a]**5:14** Law 14:7; Ay 33:25
[b]**5:15** Yos 4:24; 1Sam 17:46
[c]**5:16** Mwa 14:23; Dan 5:17
[d]**5:17** Kut 20:24
[e]**5:18** 2Fal 7:2
[f]**5:19** 1Sam 1:17; Mdo 15:33
[g]**5:20** Kut 20:7
[h]**5:22** 2Fal 5:5; Mwa 45:22
[i]22 Talanta ya fedha ni sawa na kilo 34.
[j]**5:26** 2Fal 5:16; Yer 45:5
[k]**5:27** Hes 12:10; Kut 4:6
[l]**6:1** 1Sam 10:5

anaweza kupata nguzo moja, nasi tujenge
huko mahali petu pa kuishi.”

Naye akawaambia, “Nendeni.”

3 Kisha mmoja wao akasema, “Je,
tafadhali, huwezi kufuatana na watumishi
wako?”

Elisha akajibu, “Nitakuja.” 4 Naye
akaenda pamoja nao.

Basi wakaenda Yordani, nao wakaanza
kukata miti. 5 Mmoja wao alipokuwa
anakata mti, shoka lilitumbukia kwenye
maji. Akalia, “Ee bwana wangu, shoka
lilikuwa la kuazima!”

6 [a]Mtu wa Mungu akauliza, “Je, liliangukia
wapi?” Alipomwonyesha mahali penyewe,
Elisha akakata kijiti na kukitupa mahali
pale, nalo shoka likaelea. 7 Akasema,
“Lichukue.” Kisha yule mtu akanyoosha
mkono wake, akalichukua.

### *Elisha Awanasa Waaramu Waliopofushwa*

8 Wakati huo mfalme wa Aramu
alikuwa akipigana vita na Israeli. Baada
ya kukubaliana na maafisa wake, akasema,
“Nitapiga kambi yangu mahali fulani na
fulani.”

9 [b]Mtu wa Mungu akatuma ujumbe
kwa mfalme wa Israeli: “Jihadhari usije
ukapita mahali pale, kwa sababu Waaramu
wanashuka huko.” 10 [c]Kwa hiyo mfalme wa
Israeli akatuma neno la tahadhari mahali
pale alikokuwa ameelekezwa na mtu wa
Mungu. Mara kwa mara Elisha alimwonya
mfalme kwamba watu wawe macho kwenye
maeneo kama hayo.

11 Hili lilimfadhaisha sana mfalme
wa Aramu. Akawaita maafisa wake,
akawauliza, “Je, hamtaniambia ni nani
miongoni mwenu aliye upande wa mfalme
wa Israeli?”

12 [d]Mmoja wa maafisa wake akasema,
“Mfalme bwana wangu, hakuna hata mmoja
wetu. Lakini Elisha, yule nabii aliye Israeli,
humwambia mfalme wa Israeli hata yale
maneno unayozungumza katika chumba
chako cha kulala.”

13 [e]Mfalme akaagiza akisema, “Nendeni,
mkatafute aliko, ili niweze kutuma watu
kumkamata.” Taarifa ikarudi kwamba,
“Yuko Dothani.” 14 [f]Ndipo akatuma farasi na
magari ya vita na jeshi lenye nguvu huko.
Walikwenda usiku na kuuzunguka mji.

15 Kesho yake asubuhi na mapema,
mtumishi wa mtu wa Mungu alipoamka
na kutoka nje, jeshi, pamoja na farasi na
magari ya vita, likawa limeuzunguka mji.
Mtumishi wake akasema, “Ole wetu, bwana
wangu! Tutafanya nini?”

16 [g]Nabii akajibu, “Usiogope. Wale walio
pamoja nasi ni wengi zaidi kuliko wale
walio pamoja nao.”

17 Kisha Elisha akaomba, “Ee Bwana,
mfumbue macho huyu mtumishi ili apate
kuona.” Ndipo Bwana akayafumbua macho
ya yule mtumishi, naye akatazama na
kuona vilima vimejaa farasi na magari ya
moto, yamemzunguka Elisha pande zote.

18 [h]Wakati adui waliposhuka kumwelekea,
Elisha akamwomba Bwana: “Wapige watu
hawa kwa upofu.” Basi Mungu akawapiga
kwa upofu, kama Elisha alivyoomba.

19 Elisha akawaambia, “Hii sio njia
yenyewe, na huu sio huo mji. Nifuateni
mimi, nami nitawapeleka kwa huyo
mtu mnayemtafuta.” Naye akawapeleka
Samaria.

20 Baada ya kuingia mjini, Elisha akasema,
“Bwana, yafungue macho ya watu hawa ili
wapate kuona.” Ndipo Bwana akayafungua
macho yao, na walipotazama, kumbe hapo
ndipo walipojikuta, ndani ya Samaria.

21 [i]Wakati mfalme wa Israeli alipowaona,
akamuuliza Elisha, “Je, baba yangu,
niwaue?”

22 [j]Naye akajibu, “Usiwaue. Je, utawaua
watu uliowateka kwa upanga wako
mwenyewe na upinde wako? Wape chakula
na maji ili wapate kula na kunywa, na
kisha wamrudie bwana wao.” 23 [k]Basi

[a]**6:6** Kut 15:25; 2Fal 2:21
[b]**6:9** 2Fal 6:12
[c]**6:10** Yer 11:18
[d]**6:12** 2Fal 6:9
[e]**6:13** Mwa 37:17
[f]**6:14** 2Fal 1:9
[g]**6:16** 2Nya 32:7; Za 55:18
[h]**6:18** Mwa 19:11; Mdo 13:11
[i]**6:21** 2Fal 5:13
[j]**6:22** Kum 20:11; 2Nya 28:8-15
[k]**6:23** 2Fal 5:2

akawaandalia karamu kubwa, na baada ya kula na kunywa, akawaaga nao wakarudi kwa bwana wao. Hivyo, vikosi kutoka Aramu vikakoma kuvamia nchi ya Israeli.

*Njaa Katika Samaria Iliyozingirwa*

24 [a]Baada ya kitambo kidogo, Ben-Hadadi mfalme wa Aramu akaandaa jeshi lake lote akapanda kwenda kuihusuru Samaria.
25 [b]Kukawa na njaa kuu katika mji. Samaria ilizingirwa kwa muda mrefu, kiasi kwamba kichwa cha punda kiliuzwa kwa shekeli themanini[c] za fedha, na robo ya kibaba[d] cha mavi ya njiwa kiliuzwa kwa shekeli tano[e] za fedha.

26 Wakati mfalme wa Israeli alipokuwa anapita juu ya ukuta, mwanamke mmoja akamlilia, "Bwana wangu mfalme, nisaidie!"

27 Mfalme akajibu, "Ikiwa BWANA hakusaidii, nitakutolea wapi msaada? Je, ni kutoka kwenye sakafu ya kupuria? Au kwenye shinikizo la divai?" 28 Kisha akamuuliza, "Kwani kuna nini?"

Yule mwanamke akamjibu, "Huyu mwanamke aliniambia, 'Mtoe mwanao ili tupate kumla leo, na kesho tutamla mwanangu.' 29 [f]Basi tukampika mwanangu na kumla. Siku iliyofuata nikamwambia, 'Mtoe mwanao ili tupate kumla.' Lakini akawa amemficha."

30 [g]Wakati mfalme aliposikia maneno ya yule mwanamke, alirarua mavazi yake. Naye alipoendelea kutembea ukutani, watu wakamtazama, na ndani ya mavazi yake alikuwa amevaa nguo ya gunia mwilini mwake. 31 Akasema, "Mungu na anitendee hivyo na kuzidi, ikiwa kichwa cha Elisha mwana wa Shafati kitabaki juu ya mabega yake leo!"

32 [h]Wakati huu, Elisha alikuwa ameketi ndani ya nyumba yake, akiwa pamoja na wazee. Mfalme akatuma mjumbe kumtangulia, lakini kabla hajafika, Elisha akawaambia wale wazee, "Hammwoni huyu muuaji jinsi anavyotuma mtu kukata kichwa changu? Tazama, wakati mjumbe huyo atakapofika, fungeni mlango na mzuieni asiingie. Je, vishindo vya nyayo za bwana wake haviko nyuma yake?"

33 [i]Alipokuwa angali bado anazungumza nao, mjumbe akamfikia. Naye mfalme akasema, "Maafa haya yanatoka kwa BWANA. Kwa nini niendelee kumngoja BWANA zaidi?"

7 [j]Elisha akasema, "Sikiliza neno la BWANA. Hivi ndivyo asemavyo BWANA: Wakati kama huu kesho, kipimo kimoja[k] cha unga mzuri kitauzwa kwa shekeli moja ya fedha,[l] na vibaba viwili vya shayiri kwa shekeli moja ya fedha katika lango la Samaria."

2 [m]Yule afisa ambaye mfalme alikuwa anauegemea mkono wake akamwambia yule mtu wa Mungu, "Tazama, hata kama BWANA atafungua madirisha ya mbinguni, je, jambo hili litawezekana?"

Elisha akajibu, "Utaona kwa macho yako mwenyewe, lakini wewe hutakula chochote kati ya hivyo!"

*Mwisho Wa Kuzingirwa*

3 [n]Basi kulikuwepo na watu wanne wenye ukoma katika ingilio la lango la mji. Wakaambiana, "Kwa nini tukae hapa mpaka tufe? 4 Kama tukisema, 'Tutaingia mjini,' mjini kuna njaa, nasi tutakufa humo. Kama tukikaa hapa, tutakufa. Kwa hiyo twende kwenye kambi ya Waaramu na tujisalimishe. Kama wakituacha hai, tutaishi; kama wakituua, basi na tufe."

5 Wakati wa giza la jioni, wakaondoka na kwenda kwenye kambi ya Waaramu. Walipofika mwanzo wa kambi, hapakuwa na mtu, 6 [o]kwa kuwa Bwana alililifanya jeshi

---

[a]**6:24** 1Fal 15:18; Kum 28:52
[b]**6:25** Law 26:26; Isa 36:12
[c]25 Shekeli 80 za fedha ni sawa na kilo moja.
[d]25 Robo ya kibaba ni sawa na lita 0.3.
[e]25 Shekeli tano za fedha ni sawa na gramu 55.
[f]**6:29** Law 26:29; Kum 28:53-55
[g]**6:30** Isa 22:15; Mwa 37:34
[h]**6:32** Eze 8:1; 1Fal 18:4
[i]**6:33** Ay 2:9
[j]**7:1** 2Fal 7:16
[k]1 Kipimo kimoja cha unga ni sawa na kilo 3.
[l]1 Shekeli moja ya fedha ni sawa na gramu 11.
[m]**7:2** Mwa 7:11; Mal 3:10
[n]**7:3** Law 13:45-46; Hes 5:1-4
[o]**7:6** Kut 14:24; Yer 46:21

la Waaramu lisikie sauti kama ya magari ya vita, farasi na jeshi kubwa, kiasi kwamba waliambiana, “Tazama, mfalme wa Israeli ameajiri mfalme wa Wahiti na mfalme wa Wamisri kuja kutushambulia sisi!” 7 [a]Kwa hiyo wakaondoka na kukimbia wakati wa giza la jioni na kuacha mahema yao, farasi wao na punda wao. Wakakimbia kuokoa maisha yao na kuacha kila kitu ndani ya kambi kama kilivyokuwa.

8 [b]Wale watu wenye ukoma walipofika mwanzoni mwa kambi, wakaingia kwenye mojawapo ya mahema. Wakala na kunywa, na kuchukua fedha, dhahabu na nguo, wakaenda kuvificha. Wakarudi na kuingia katika hema jingine, na kuchukua baadhi ya vitu kutoka ndani yake na kuvificha pia.

9 Kisha wakaambiana, “Hili tunalolifanya sio jema. Hii ni siku ya habari njema, nasi tunakaa kimya. Kama tukisubiri mpaka mapambazuko, maafa yatatupata. Twendeni mara moja tukatoe habari hizi katika jumba la mfalme.”

10 Hivyo wakaenda mjini na kuwaita walinzi wa langoni, wakawaambia, “Tulikwenda katika kambi ya Waaramu lakini hapakuwepo na mtu huko, hata sauti ya mtu yeyote, ila farasi na punda waliofungwa na mahema yaliyoachwa kama yalivyokuwa.” 11 Walinzi wa langoni wakatangaza habari ile kwa sauti kuu, na taarifa hii ikatolewa ndani ya jumba la mfalme.

12 [c]Mfalme akaamka usiku na kuwaambia maafisa wake, “Nitawaambia kile Waaramu walichotufanyia. Wanajua kwamba tuna njaa, hivyo wameacha kambi yao ili kujificha mashambani, wakifikiri, ‘Kwa hakika watatoka nje ya mji, nasi tutawakamata wakiwa hai na kuingia ndani ya mji.’ ”

13 Mmoja wa maafisa wake akajibu, “Waamuru watu wachache wakawachukue farasi watano kati ya wale waliobaki katika mji. Hatima yao itakuwa kama ya Waisraeli wote walio hapa. Watakuwa tu kama Waisraeli hawa ambao wanangoja kifo. Hivyo tuwatumeni wajue kumetendeka nini.”

14 Ndipo wakachagua magari mawili ya vita pamoja na farasi wake, naye mfalme akawatuma wafuatilie jeshi la Waaramu. Akawaamuru waendeshaji akisema, “Nendeni mkaone ni nini kilichotokea.” 15 Wakawafuatia hadi Yordani, nao wakakuta barabara yote ikiwa imetapakaa nguo na vyombo vya Waaramu walivyokuwa wamevitupa walipokuwa wanatoroka. Basi wale wajumbe wakarudi na kutoa taarifa kwa mfalme. 16 [d]Kisha watu wakatoka na kuteka nyara kambi ya Waaramu. Kwa hiyo kipimo cha unga mzuri kikauzwa kwa shekeli, na vipimo viwili vya shayiri kwa shekeli, kama vile Bwana alivyokuwa amesema.

17 [e]Basi mfalme alikuwa amemweka yule afisa ambaye mfalme alikuwa anauegemea mkono wake awe msimamizi wa lango. Nao watu wakamkanyaga walipoingia langoni, naye akafa, kama vile mtu wa Mungu alivyokuwa ametangulia kusema wakati mfalme alipofika nyumbani kwake. 18 Ikatokea kama vile mtu wa Mungu alivyokuwa amemwambia mfalme: “Wakati kama huu kesho, kipimo kimoja cha unga mzuri kitauzwa kwa shekeli moja ya fedha, na vibaba viwili vya shayiri kwa shekeli moja ya fedha katika lango la Samaria.”

19 [f]Yule afisa alikuwa amemwambia yule mtu wa Mungu, “Tazama, hata kama Bwana atafungua madirisha ya mbinguni, je, jambo hili litawezekana?” Naye yule mtu wa Mungu alikuwa amemjibu, “Utaona kwa macho yako mwenyewe, lakini wewe hutakula chochote kati ya hivyo!” 20 Ndivyo hasa ilivyotokea kwake, kwa kuwa watu walimkanyaga langoni, naye akafa.

### *Ardhi Ya Mshunami Yarudishwa*

8 [g]Wakati huu, Elisha alikuwa amemwambia yule mwanamke ambaye mwanawe alikuwa amefufuliwa, “Ondoka wewe na jamaa yako ukaishi mahali

---

[a]**7:7** Za 48:4-6; Mit 28:1
[b]**7:8** Isa 33:23
[c]**7:12** Yos 8:4
[d]**7:16** Isa 33:4
[e]**7:17** 2Fal 7:2
[f]**7:19** 2Fal 7:2
[g]**8:1** 2Fal 4:8-37; Kum 28:22

popote unapoweza kwa kitambo kidogo,
kwa sababu Bwana ameamuru njaa katika
nchi hii ambayo itadumu kwa miaka saba."
2 Yule mwanamke akafanya kama vile yule
mtu wa Mungu alivyosema. Yeye na jamaa
yake wakaondoka na kwenda kuishi katika
nchi ya Wafilisti kwa miaka saba.
3 Baada ya miaka saba, yule mwanamke
akarudi kutoka nchi ya Wafilisti, akaenda
kwa mfalme kumsihi kwa ajili ya nyumba
yake na shamba lake. 4 Mfalme alikuwa
anazungumza na Gehazi, mtumishi wa
mtu wa Mungu, naye alikuwa amesema,
"Hebu niambie mambo yote makuu
yaliyofanywa na Elisha." 5 [a]Wakati Gehazi
alipokuwa akimweleza mfalme jinsi Elisha
alivyomfufua mtu, yule mwanamke ambaye
mwanawe alikuwa amefufuliwa na Elisha
akaja ili amsihi mfalme kwa ajili ya nyumba
yake na shamba lake.

Gehazi akasema, "Huyu ndiye huyo mwanamke, bwana wangu mfalme, na huyu ndiye mwanawe ambaye Elisha alimfufua."
6 Mfalme akamuuliza yule mwanamke
kuhusu mambo hayo, naye akamweleza.

Ndipo akaamuru afisa ashughulikie shauri lake na kumwambia, "Mrudishie huyu mwanamke kila kitu kilichokuwa mali yake, pamoja na mapato yote yaliyotokana na shamba lake tangu siku alipoondoka nchini hadi sasa."

*Hazaeli Anamuua Ben-Hadadi*

7 [b]Elisha akaenda Dameski, naye Ben-
Hadadi mfalme wa Aramu alikuwa
mgonjwa. Mfalme alipoambiwa, "Mtu
wa Mungu ametoka mbali akapanda hadi
hapa," 8 [c]mfalme akamwambia Hazaeli.
"Chukua zawadi na uende kumlaki huyo mtu wa Mungu. Muulize Bwana kupitia yeye, kwamba, 'Je, nitapona ugonjwa huu?' "

9 Hazaeli akaenda kumlaki Elisha, akiwa amechukua zawadi ya kila kitu kizuri kilichopatikana Dameski, mizigo iliyobebwa na ngamia arobaini. Akaingia ndani na kusimama mbele yake, akasema, "Mwanao Ben-Hadadi mfalme wa Aramu amenituma niulize, 'Je, nitapona ugonjwa huu?' "

10 Elisha akajibu, "Nenda ukamwambie,
'Hakika utapona'; lakini Bwana
amenifunulia kwamba kweli atakufa."
11 [d]Elisha akamkazia Hazaeli macho kwa
nguvu mpaka akaona aibu. Kisha mtu wa
Mungu akaanza kulia.

12 [e]Hazaeli akauliza "Kwa nini bwana wangu analia?"

Elisha akajibu, "Kwa sababu najua mabaya utakayowatendea Waisraeli. Utachoma moto ngome zao, utawaua vijana wao kwa upanga, kuwatupa chini kwa nguvu watoto wachanga, na kuwatumbua wanawake wenye mimba."

13 [f]Hazaeli akasema, "Itawezekanaje mtumishi wako, aliye mbwa tu, kufanya tendo la ajabu namna hiyo?"

Elisha akamjibu, "Bwana amenionyesha kuwa utakuwa mfalme wa Aramu."

14 Kisha Hazaeli akamwacha Elisha
na kumrudia bwana wake. Ben-Hadadi
akamuuliza, "Elisha alikuambia nini?"
Hazaeli akajibu, "Aliniambia kwamba
hakika utapona." 15 [g]Lakini kesho yake
Hazaeli akachukua nguo nzito, akailoweka ndani ya maji, akaitandaza juu ya uso wa mfalme, hivyo akafa. Kisha Hazaeli akaingia mahali pake kuwa mfalme wa Aramu.

*Yehoramu Mfalme Wa Yuda*

**(2 Nyakati 21:1-20)**

16 [h]Katika mwaka wa tano wa Yoramu
mwana wa Ahabu mfalme wa Israeli,
wakati huo Yehoshafati akiwa mfalme wa
Yuda, Yehoramu mwana wa Yehoshafati
akaanza kutawala kama mfalme wa Yuda.
17 Alikuwa na umri wa miaka thelathini na
miwili alipoanza kutawala, naye akatawala
huko Yerusalemu kwa miaka minane.
18 Akaenenda katika njia za wafalme wa
Israeli, kama nyumba ya Ahabu ilivyokuwa
imefanya, kwa kuwa alimwoa binti wa

[a]**8:5** 2Fal 4:35
[b]**8:7** 2Sam 8:5; 2Fal 6:27
[c]**8:8** 1Fal 19:15; 1Sam 9:7
[d]**8:11** Lk 19:41; Amu 3:25
[e]**8:12** 1Fal 19:17; 2Fal 15:16
[f]**8:13** 1Sam 17:43; 1Fal 19:15
[g]**8:15** 2Fal 1:17
[h]**8:16** 2Fal 1:17; 2Nya 21:1-4

Ahabu. Akatenda maovu machoni pa
BWANA. 19 [a]Hata hivyo, kwa ajili ya
Daudi mtumishi wake, BWANA hakutaka
kuiangamiza Yuda. Alikuwa ameahidi
kuidumisha taa kwa ajili ya Daudi na wazao
wake milele.

20 [b]Wakati wa Yehoramu, Edomu waliasi
dhidi ya Yuda na kujiwekea mfalme wao
wenyewe. 21 Basi Yehoramu akaenda
Sairi pamoja na magari yake yote ya
vita. Waedomu wakamzunguka yeye na
majemadari wake wa magari yake ya
vita, lakini akaondoka, akapenya usiku na
kuwashambulia Waedomu. Hata hivyo,
jeshi lake likatorokea nyumbani mwao.
22 [c]Hadi leo Edomu wameasi dhidi ya Yuda.
Libna pia wakaasi wakati huo huo.

23 Kwa matukio mengine ya utawala
wa Yehoramu na yote aliyoyafanya,
je, hayakuandikwa katika kitabu cha
kumbukumbu za wafalme wa Yuda?
24 Yehoramu akalala pamoja na baba
zake, na akazikwa pamoja nao katika Mji
wa Daudi. Naye Ahazia mwanawe akawa
mfalme baada yake.

*Ahazia Mfalme Wa Yuda*

**(2 Nyakati 22:1-6)**

25 [d]Katika mwaka wa kumi na mbili wa
utawala wa Yoramu mwana wa Ahabu
mfalme wa Israeli, Ahazia mwana wa
Yehoramu mfalme wa Yuda alianza
kutawala. 26 [e]Ahazia alikuwa na umri
wa miaka ishirini na miwili alipoanza
kutawala, naye akatawala katika
Yerusalemu kwa mwaka mmoja. Mama
yake aliitwa Athalia, mjukuu wa Omri
mfalme wa Israeli. 27 [f]Akaenenda katika
njia za nyumba ya Ahabu, na kutenda
maovu machoni pa BWANA, kama nyumba
ya Ahabu ilivyokuwa imefanya, kwa kuwa
alikuwa ameoa kutoka nyumba ya Ahabu.

28 [g]Ahazia akaenda vitani na Yoramu

[a]**8:19** 2Sam 21:17
[b]**8:20** 1Fal 22:47
[c]**8:22** Mwa 27:40; Yos 21:13
[d]**8:25** 2Fal 9:29
[e]**8:26** 2Fal 8:18; 1Fal 16:23
[f]**8:27** 1Fal 16:30; 15:26
[g]**8:28** Kum 4:43; 2Fal 9:1, 14

mwana wa Ahabu kupigana na Hazaeli
mfalme wa Aramu huko Ramoth-Gileadi.
Waaramu wakamjeruhi Yoramu. 29 [h]Hivyo
Mfalme Yoramu akarudi Yezreeli ili apate
kuuguza majeraha aliyojeruhiwa na
Waaramu huko Ramothi[i] alipopigana na
Hazaeli mfalme wa Aramu.

Ndipo Ahazia mwana wa Yehoramu
mfalme wa Yuda akashuka kwenda Yezreeli
kumtazama Yoramu mwana wa Ahabu, kwa
sababu alikuwa amejeruhiwa.

*Yehu Atiwa Mafuta Kuwa Mfalme*

9 [j]Nabii Elisha akamwita mtu mmoja
kutoka kwa wana wa manabii na
kumwambia, "Jikaze viuno, uichukue hii
chupa ya mafuta, na uende Ramoth-Gileadi.
2 Ukifika huko, mtafute Yehu mwana wa
Yehoshafati, mwana wa Nimshi. Enda
kwake, umtenge na wenzake, na umpeleke
katika chumba cha ndani. 3 [k]Kisha chukua
hii chupa na umimine mafuta juu ya
kichwa chake, nawe utangaze, 'Hivi ndivyo
asemavyo BWANA: Ninakutia mafuta uwe
mfalme juu ya Israeli.' Kisha ufungue
mlango na ukimbie; usikawie!"

4 Basi yule kijana nabii akaenda Ramoth-
Gileadi. 5 Wakati alipofika, akawakuta
maafisa wa jeshi wameketi pamoja,
akasema, "Nina ujumbe wako, ee jemadari."

Yehu akauliza, "Kwa yupi miongoni
mwetu?"

Akamjibu, "Kwako wewe, jemadari."

6 [l]Yehu akainuka na kuingia ndani ya
nyumba. Ndipo yule nabii akamimina
mafuta juu ya kichwa cha Yehu na
kutangaza, "Hivi ndivyo asemavyo BWANA,
Mungu wa Israeli: 'Ninakutia mafuta uwe
mfalme juu ya watu wa BWANA, yaani
Israeli. 7 [m]Inakupasa uiangamize nyumba ya
bwana wako Ahabu, nami nitalipiza kisasi
cha damu ya watumishi wangu manabii
na damu ya watumishi wote wa BWANA

[h]**8:29** 1Fal 21:29; 2Fal 10:13
[i]29 Yaani Rama kwa Kiebrania.
[j]**9:1** 1Sam 10:5; 2Fal 8:28
[k]**9:3** 1Fal 19:16
[l]**9:6** 1Fal 19:16
[m]**9:7** Mwa 4:24; Kum 32:43

iliyomwagwa na Yezebeli. 8 [a]Nyumba yote ya
Ahabu itaangamia. Nitamkatilia mbali kila
mzaliwa wa kiume wa Ahabu katika Israeli,
aliye mtumwa ama aliye huru. 9 [b]Nitaifanya
nyumba ya Ahabu kuwa kama ile nyumba
ya Yeroboamu mwana wa Nebati, na kama
ile nyumba ya Baasha mwana wa Ahiya.
10 [c]Kuhusu Yezebeli, mbwa watamla kwenye
kiwanja huko Yezreeli, wala hakuna mtu
atakayemzika.' " Kisha akafungua mlango
na kukimbia.

11 [d]Yehu alipotoka nje na kurudi kwenda
kwa maafisa wenzake, mmoja wao
akamuuliza, "Je, kila kitu ni salama? Kwa
nini huyu mwenye wazimu alikuja kwako?"

Yehu akajibu, "Wewe unamfahamu
huyo mtu, na aina ya mambo ambayo yeye
husema."

12 Wakasema, "Hiyo siyo kweli! Tuambie."

Yehu akasema, "Haya ndiyo aliyoniambia:
'Hivi ndivyo asemavyo BWANA: Ninakutia
mafuta uwe mfalme juu ya Israeli.' "

13 [e]Wakaharakisha kuvua mavazi yao, na
kuyatandaza chini ya Yehu ili akanyage
juu kwenye ngazi ya nje. Kisha wakapiga
tarumbeta na kupaza sauti wakisema,
"Yehu ni mfalme!"

*Yehu Anamuua Yoramu Na Ahazia*

14 [f]Basi Yehu mwana wa Yehoshafati,
mwana wa Nimshi, akafanya shauri baya
dhidi ya Yoramu. (Wakati huu, Yoramu
na Israeli wote walikuwa wakiilinda
Ramoth-Gileadi dhidi ya Hazaeli mfalme
wa Aramu, 15 [g]lakini Mfalme Yoramu
alikuwa amerudishwa Yezreeli ili kujiuguza
kutokana na majeraha ambayo Waaramu
walimtia katika vita na Hazaeli mfalme wa
Aramu.) Yehu akasema, "Kama hii ndiyo
nia yenu, msimruhusu hata mmoja kutoroka
nje ya mji kwenda kupeleka habari huko
Yezreeli." 16 [h]Ndipo Yehu akaingia katika
gari lake la vita na kuendesha kwenda
Yezreeli, kwa sababu Yoramu alikuwa
amepumzika huko, na Ahazia mfalme wa
Yuda alikuwa ameenda kumwona.

17 [i]Mlinzi aliyesimama juu ya kinara cha
Yezreeli alipoona askari wa Yehu wanakuja,
akaita akisema, "Naona askari wanakuja."

Yoramu akaamuru, "Mtwae mpanda
farasi umtume akakutane nao na kuuliza,
'Je, mmekuja kwa amani?' "

18 Mpanda farasi akaondoka kwenda
kukutana na Yehu na kusema, "Hivi
ndivyo asemavyo mfalme: 'Je, mmekuja
kwa amani?' "

Yehu akamjibu, "Una nini na amani?
Unga msafara nyuma yangu."

Mlinzi akatoa habari, "Mjumbe
amewafikia lakini harudi."

19 Basi mfalme akamtuma mpanda farasi
wa pili. Wakati alipowafikia akasema, "Hivi
ndivyo asemavyo mfalme, 'Je, mmekuja
kwa amani?' "

Yehu akajibu, "Una nini na amani? Unga
msafara nyuma yangu."

20 [j]Yule mlinzi akatoa taarifa akasema,
"Mjumbe amewafikia, lakini hata yeye
harudi. Uendeshaji ule ni kama wa Yehu
mwana wa Nimshi, anaendesha kama
mwenye wazimu!"

21 [k]Yoramu akaagiza, akasema, "Weka
tayari gari langu la vita." Na baada ya gari
kuwa tayari, Yoramu mfalme wa Israeli,
na Ahazia mfalme wa Yuda, wakaondoka
kila mmoja kwenye gari lake ili kukutana
na Yehu. Walikutana naye katika shamba
lililokuwa mali ya Nabothi, Myezreeli.
22 [l]Yoramu alipomwona Yehu akauliza, "Je,
Yehu, umekuja kwa amani?"

Yehu akajibu, "Kunawezaje kuwa na
amani wakati ibada za sanamu na uchawi
wa mama yako Yezebeli ungaliko?"

23 [m]Yoramu akageuka nyuma na kukimbia,
akimwambia Ahazia, "Huu ni uhaini,
Ahazia!"

---

[a]**9:8** 1Sam 25:22
[b]**9:9** 1Fal 14:10
[c]**9:10** 1Fal 21:23
[d]**9:11** Yn 10:20; 1Sam 10:11
[e]**9:13** Mt 21:8; 2Sam 15:10
[f]**9:14** Kum 4:43; 2Fal 8:28
[g]**9:15** 2Fal 8:29
[h]**9:16** 2Nya 22:7
[i]**9:17** 1Sam 14:16
[j]**9:20** 2Sam 18:27
[k]**9:21** 1Fal 21:1
[l]**9:22** 1Fal 18:19
[m]**9:23** 2Fal 11:14

24 [a]Kisha Yehu akatwaa upinde wake na
kumchoma Yoramu katikati ya mabega.
Mshale ukapenya kwenye moyo wake,
naye akaanguka ghafula ndani ya gari
lake. 25 [b]Yehu akamwambia Bidkari,
mwendeshaji wa gari lake, “Mwinue na
umtupe katika shamba lililokuwa mali
ya Nabothi, Myezreeli. Kumbuka jinsi
mimi na wewe tulivyokuwa tukiendesha
pamoja magari yetu nyuma ya Ahabu
baba yake, wakati BWANA alipotoa unabii
huu kumhusu: 26 [c]‘Jana niliona damu ya
Nabothi na damu ya wanawe, nami kwa
hakika nitakufanya uilipe juu ya shamba
hili, asema BWANA.’ Sasa basi, mwinue na
umtupe juu ya kiwanja, kulingana na neno
la BWANA.”

27 [d]Wakati Ahazia mfalme wa Yuda
alipoona kilichotokea, akakimbia
kupitia barabara ya Beth-Hagani. Yehu
akamkimbiza akipaza sauti na kusema,
“Muue naye pia!” Wakamjeruhi katika gari
lake kwenye njia ielekeayo Guri karibu na
Ibleamu, lakini akatorokea Megido na akafia
huko. 28 [e]Watumishi wake wakambeba kwa
gari la vita na kumpeleka Yerusalemu,
wakamzika pamoja na baba zake kwenye
kaburi lake katika Mji wa Daudi. 29 [f](Katika
mwaka wa kumi na moja wa Yoramu
mwana wa Ahabu, Ahazia alianza kutawala
katika Yuda.)

*Yezebeli Auawa*

30 [g]Kisha Yehu akaenda Yezreeli. Yezebeli
aliposikia habari hii, akayapaka macho
yake rangi, akatengeneza nywele zake na
kutazama nje dirishani. 31 [h]Yehu alipokuwa
akiingia langoni, Yezebeli akasema, “Je,
umekuja kwa amani, Zimri, wewe muuaji
wa bwana wako?”

32 Yehu akaangalia juu dirishani na
kuita, “Je, ni nani aliye upande wangu?
Ni nani?” Matowashi wawili au watatu
wakamtazama. 33 [i]Yehu akasema, “Mtupeni
huyo mwanamke chini!” Kwa hiyo
wakamtupa chini, nayo baadhi ya damu
yake ikatapanyika ukutani na nyingine juu
ya farasi walipokuwa wakimkanyaga kwa
miguu yao.

34 [j]Yehu akaingia ndani, akala na
akanywa. Akasema, “Mshughulikieni huyo
mwanamke aliyelaaniwa. Mzikeni, kwa
sababu alikuwa binti wa mfalme.” 35 Lakini
walipotoka kwenda kumzika, hawakukuta
kitu chochote isipokuwa fuvu la kichwa,
miguu yake na mikono. 36 [k]Wakarudi na
kumwambia Yehu, ambaye alisema, “Hili
ndilo neno la BWANA alilosema kupitia
kinywa cha mtumishi wake Eliya Mtishbi,
kwamba: Katika kiwanja cha Yezreeli,
mbwa wataikula nyama ya Yezebeli.
37 [l]Maiti ya Yezebeli itakuwa kama mavi
shambani katika uwanja wa Yezreeli,
kwamba hakutakuwepo mtu atakayeweza
kusema, ‘Huyu ndiye Yezebeli.’ ”

*Jamii Ya Ahabu Yauawa*

10 [m]Wakati huu katika Samaria
walikuwepo wana sabini wa nyumba
ya Ahabu. Kwa hiyo Yehu akaandika barua
na kuzituma Samaria: kwa maafisa wa
Yezreeli, kwa wazee, na kwa walezi wa
watoto wa Ahabu. Akasema, 2 “Mara tu
barua hii itakapokufikia, kwa kuwa wana
wa bwana wako wapo pamoja nawe, nawe
una magari ya vita na farasi, mji wenye
ngome na silaha, 3 mchague mwenye
uwezo zaidi kati ya wana wa bwana wako,
na umweke juu ya kiti cha enzi cha baba
yake. Kisha upigane kwa ajili ya nyumba
ya bwana wako.”

4 Lakini wakaogopa sana na kusema,
“Ikiwa wafalme wawili hawakuweza
kupambana na Yehu, sisi tutawezaje?”

5 [n]Basi msimamizi wa jumba la mfalme,
mtawala wa mji, na wazee na walezi

[a]**9:24** 1Fal 22:34
[b]**9:25** 1Fal 21:19-22
[c]**9:26** 1Fal 21:19
[d]**9:27** Amu 1:27; 2Fal 23:29
[e]**9:28** 2Fal 23:30
[f]**9:29** 2Fal 8:25
[g]**9:30** Yer 4:30; Eze 23:40
[h]**9:31** 1Fal 16:9-10
[i]**9:33** Za 7:5
[j]**9:34** 1Fal 16:31
[k]**9:36** Za 68:23; 1Fal 21:23
[l]**9:37** Za 83:10; Yer 8:2
[m]**10:1** 1Fal 13:32; Amu 8:30
[n]**10:5** Yos 9:8

wakatuma ujumbe huu kwa Yehu: "Sisi
tu watumishi wako, na tutafanya kila kitu
utakachosema. Hatutamteuwa mtu yeyote
kuwa mfalme. Wewe fanya uonalo kuwa
ni bora."
6 Kisha Yehu akawaandikia barua ya pili,
akisema, "Ikiwa ninyi mko upande wangu
na mtanitii mimi, twaeni vichwa vya wana
wa bwana wenu, na mnijie huku Yezreeli
kesho wakati kama huu."
Wakati huo wana sabini wa mfalme
walikuwa wakiishi pamoja na viongozi
wa mji wa Samaria, waliokuwa wakiwalea.
7 [a]Hiyo barua ilipowafikia, watu hawa
wakawachukua wale wana sabini wa
mfalme na kuwachinja wote. Wakaweka
vichwa vyao ndani ya makapu na
kumpelekea Yehu huko Yezreeli. 8 Mjumbe
alipofika, akamwambia Yehu, "Wameleta
vichwa vya wana wa mfalme."
Ndipo Yehu akaagiza, "Viwekeni
malundo mawili katika ingilio la lango la
mji mpaka asubuhi."
9 Asubuhi yake, Yehu akatoka nje.
Akasimama mbele ya watu wote na akasema,
"Hamna hatia. Ni mimi niliyefanya shauri
baya dhidi ya bwana wangu na kumuua,
lakini ni nani aliyewaua wote hawa?
10 [b]Fahamuni basi kwamba, hakuna neno
ambalo BWANA amesema dhidi ya nyumba
ya Ahabu ambalo halitatimia. BWANA
amefanya lile aliloahidi kupitia mtumishi
wake Eliya." 11 Hivyo Yehu akaua kila
mtu huko Yezreeli aliyekuwa amebaki
wa nyumba ya Ahabu, ikiwa ni pamoja
na wakuu wake, rafiki zake wa karibu,
na makuhani wake. Hakuacha yeyote
anusurike.
12 Kisha Yehu akaondoka kuelekea
Samaria. Alipokuwa njiani karibu na
nyumba ya kukatia manyoya ya kondoo,
yaani, Beth-Ekedi ya wachunga kondoo,
13 [c]Yehu akakutana na watu wa jamaa ya
Ahazia mfalme wa Yuda, akauliza, "Ninyi
ni nani?"
Wao wakasema, "Sisi ni jamaa ya Ahazia,
nasi tumeshuka kuwasalimu jamaa ya
mfalme na ya mama malkia."
14 [d]Yehu akaagiza, "Wakamateni wakiwa
hai!" Kwa hiyo wakawachukua wakiwa hai,
watu arobaini na wawili, na kuwachinja
kando ya kisima cha Beth-Ekedi. Hakuacha
yeyote anusurike.
15 [e]Baada ya kuondoka hapo, alimkuta
Yehonadabu mwana wa Rekabu, aliyekuwa
akienda kumlaki. Yehu akamsalimu na
kusema, "Je, moyo wako ni mnyofu kwangu
kama moyo wangu ulivyo kwako?"
Yehonadabu akajibu, "Ndiyo."
Yehu akasema, "Kama ndivyo, nipe
mkono wako." Yeye akampa mkono, naye
Yehu akampandisha kwenye gari lake la
vita. 16 [f]Yehu akasema, "Twende pamoja
ukaone wivu wangu kwa ajili ya BWANA."
Hivyo wakasafiri pamoja kwenye gari lake.
17 [g]Yehu alipofika Samaria, akawaua wale
wote waliokuwa wamesalia wa jamaa ya
Ahabu, akawaangamiza, sawasawa na neno
la BWANA alilosema kupitia Eliya.

*Watumishi Wa Baali Wauawa*

18 [h]Kisha Yehu akawaleta watu wote
pamoja na kuwaambia, "Ahabu alimtumikia
Baali kidogo. Lakini Yehu atamtumikia
zaidi. 19 [i]Sasa waiteni manabii wote wa
Baali, watumishi wake wote na makuhani
wake wote. Hakikisheni kwamba hakuna
hata mmoja atakayekosekana, kwa sababu
ninakwenda kutoa kafara kubwa sana
kwa Baali. Yeyote atakayeshindwa kuja
hataendelea kuishi." Lakini Yehu alifanya
hivyo kwa hila ili apate kuwaangamiza
watumishi wote wa Baali.
20 [j]Yehu akasema, "Itisheni kusanyiko
kwa heshima ya Baali." Basi wakatangaza
jambo hilo. 21 Kisha Yehu akapeleka ujumbe
katika Israeli yote, nao watumishi wote wa
Baali wakaja, hakuna hata mmoja ambaye
hakufika. Wakasongana ndani ya hekalu

---

[a]**10:7** 1Fal 21:21; 2Sam 4:8
[b]**10:10** 2Fal 9:7-10; 1Fal 21:29
[c]**10:13** 2Fal 8:29; 2Nya 22:8
[d]**10:14** 2Fal 10:11
[e]**10:15** Yer 35:6, 14-19; 1Nya 2:55; Ezr 10:19
[f]**10:16** Hes 25:13
[g]**10:17** 2Fal 9:8
[h]**10:18** Amu 2:11
[i]**10:19** 1Fal 18:19
[j]**10:20** Kut 32:5

la Baali hadi likajaa tangu mlango hadi
mwisho wake. 22 Naye Yehu akamwambia
yule aliyekuwa mtunza chumba cha mavazi,
“Leta majoho kwa ajili ya watumishi wote
wa Baali.” Basi akawaletea majoho.
23 Kisha Yehu na Yehonadabu mwana wa
Rekabu wakaingia ndani ya hekalu la Baali.
Yehu akawaambia watumishi wa Baali,
“Tazameni kila mahali mhakikishe kwamba
hakuna hata mtumishi mmoja wa BWANA
aliye hapa pamoja nanyi, ila ni watumishi
wa Baali tu.” 24 [a]Kwa hiyo wakaingia ndani
ili kutoa kafara na sadaka ya kuteketezwa.
Wakati huu, Yehu alikuwa amewaweka
watu wake themanini akiwa amewapa onyo
kwamba, “Ikiwa mmoja wenu atamwachia
mtu yeyote ninayemweka mikononi mwake
atoroke, itakuwa uhai wako kwa uhai
wake.”
25 [b]Mara baada ya Yehu kutoa sadaka
ya kuteketezwa, akawaamuru walinzi na
maafisa: “Ingieni ndani, waueni; asitoroke
hata mmoja.” Basi wakawakatakata kwa
upanga. Walinzi na maafisa wakazitupa zile
maiti nje, kisha wakaingia mahali pa ndani
pa kuabudia miungu katika hekalu la Baali.
26 [c]Wakaileta ile nguzo ya kuabudiwa nje
ya hekalu la Baali, na wakaichoma moto.
27 Wakabomoa ile nguzo ya kuabudiwa ya
Baali pamoja na hekalu la Baali, nao watu
wakapafanya kuwa choo hadi leo.
28 Kwa hiyo Yehu akaangamiza kuabudiwa
kwa Baali katika Israeli. 29 [d]Hata hivyo, Yehu
hakuziacha dhambi za Yeroboamu mwana
wa Nebati, ambazo alikuwa amesababisha
Israeli kuzitenda, yaani kuabudu ndama za
dhahabu huko Betheli ya Dani.
30 [e]BWANA akamwambia Yehu, “Kwa
kuwa umefanya vyema kwa kutimiza yaliyo
sawa machoni pangu, na umetenda kwa
nyumba ya Ahabu yale yote niliyokuwa
nimekusudia kutenda, wazao wako
wataketi juu ya kiti cha enzi cha Israeli hadi
kizazi cha nne.” 31 [f]Lakini Yehu hakuwa
mwangalifu kushika sheria za BWANA,
Mungu wa Israeli, kwa moyo wake wote.
Hakuziacha dhambi za Yeroboamu, ambazo
alikuwa amesababisha Israeli kuzitenda.
32 [g]Katika siku hizo, BWANA akaanza
kupunguza ukubwa wa Israeli. Hazaeli
akawashinda Waisraeli sehemu zote za nchi
yao 33 [h]mashariki ya Yordani, katika nchi
yote ya Gileadi (eneo la Gadi, Reubeni na
Manase), kutoka Aroeri karibu na Bonde la
Arnoni kupitia Gileadi hadi Bashani.
34 Kwa matukio mengine ya utawala wa
Yehu, yote aliyofanya na mafanikio yake
yote, je, hayakuandikwa katika kitabu cha
kumbukumbu za wafalme wa Israeli?
35 Yehu akalala pamoja na baba zake,
naye akazikwa huko Samaria. Naye
Yehoahazi mwanawe akawa mfalme baada
yake. 36 Muda Yehu aliotawala juu ya Israeli
huko Samaria ilikuwa miaka ishirini na
minane.

*Athalia Na Yoashi*

**(2 Nyakati 22:10–23:21)**

11 [i]Wakati Athalia mamaye Ahazia
alipoona kuwa mwanawe amekufa,
akainuka na kuiangamiza jamaa yote ya
mfalme. 2 [j]Lakini Yehosheba, binti wa
Mfalme Yehoramu, aliyekuwa pia dada
yake Ahazia, akamtwaa Yoashi mwana
wa Ahazia kwa siri kutoka miongoni
mwa wana wa mfalme waliokuwa karibu
kuuawa. Akamweka Yoashi pamoja na
yaya wake ndani ya chumba cha kulala
na kumficha humo ili Athalia asimwone;
kwa hiyo hakuuawa. 3 Alibaki amefichwa
pamoja na yaya wake katika Hekalu la
BWANA kwa muda wa miaka sita wakati
Athalia alikuwa akitawala nchi.
4 [k]Katika mwaka wa saba, Yehoyada
akatumania wakuu wa vikundi vya mamia,
na Wakari,[l] na walinzi, nao wakaletwa
kwake katika Hekalu la BWANA. Alifanya

[a]**10:24** Yos 2:14
[b]**10:25** Kut 22:20; 1Fal 18:40
[c]**10:26** Kut 23:24
[d]**10:29** 1Fal 12:30; Kut 32:4
[e]**10:30** 2Fal 15:12
[f]**10:31** Kum 4:9; Mit 4:23
[g]**10:32** Za 107:39
[h]**10:33** Hes 32:34; Isa 17:2
[i]**11:1** 2Fal 8:18
[j]**11:2** 2Fal 12:1
[k]**11:4** 2Fal 11:19
[l]4 Yaani Wakerethi (ona 1Sam 30:14; Eze 25:16; Sef 2:5, 6).

agano nao na kuwaapisha katika Hekalu
la BWANA. Ndipo akawaonyesha mwana
wa mfalme. 5 [a]Akawaamuru akisema, “Hivi
ndivyo iwapasavyo kufanya: Ninyi ambao
mko makundi matatu mnaoingia zamu
siku ya Sabato, theluthi yenu inayolinda
jumba la kifalme, 6 theluthi nyingine Lango
la Suri, na theluthi nyingine lango lililo
nyuma ya walinzi, ambao hupeana zamu
kulinda Hekalu, 7 nanyi ambao mko katika
makundi mengine mawili ambao kwa
kawaida hupumzika Sabato, wote mtalinda
Hekalu kwa ajili ya mfalme. 8 Jipangeni
kumzunguka mfalme, kila mtu akiwa na
silaha yake mkononi. Yeyote anayesogelea
safu zenu lazima auawe. Kaeni karibu na
mfalme popote aendapo.”

9 Wakuu wa vikosi vya mamia wakafanya
kama vile kuhani Yehoyada aliagiza. Kila
mmoja akawachukua watu wake, wale
waliokuwa wakiingia zamu siku ya Sabato
na wale waliokuwa wakienda mapumziko,
nao wakaja kwa kuhani Yehoyada. 10 [b]Ndipo
akawapa wale wakuu mikuki na ngao
zilizokuwa za Mfalme Daudi, zilizokuwa
ndani ya Hekalu la BWANA. 11 Wale walinzi,
kila mmoja akiwa na silaha yake mkononi
mwake, wakajipanga kumzunguka mfalme,
karibu na madhabahu na Hekalu, kuanzia
upande wa kusini hadi upande wa kaskazini
mwa Hekalu.

12 [c]Yehoyada akamtoa mwana wa mfalme
na kumvika taji, akampa nakala ya agano,
na kumtangaza kuwa mfalme. Wakamtia
mafuta, nao watu wakapiga makofi na
kupaza sauti, wakisema, “Mfalme aishi
maisha marefu!”

13 Athalia aliposikia kelele iliyofanywa
na walinzi pamoja na watu, akawaendea
watu pale penye Hekalu la BWANA.
14 [d]Akaangalia, na tazama alikuwako
mfalme, akiwa amesimama karibu na
nguzo, kama ilivyokuwa desturi. Maafisa na
wapiga tarumbeta walikuwa pembeni mwa
mfalme, nao watu wote wa nchi walikuwa
wakifurahi na kupiga tarumbeta. Ndipo
Athalia akararua mavazi yake na kulia,
“Uhaini! Uhaini!”

15 Kuhani Yehoyada akawaagiza
majemadari wa vikosi vya mamia,
waliokuwa viongozi wa jeshi, “Mleteni
nje kati ya safu, na mkamuue kwa upanga
yeyote anayemfuata.” Kwa kuwa kuhani
alikuwa amesema, “Hatauawa ndani ya
Hekalu la BWANA.” 16 Basi wakamkamata
Athalia, na alipofika mahali ambapo farasi
huingilia katika viwanja vya jumba la
mfalme, wakamuulia hapo.

17 [e]Kisha Yehoyada akafanya agano kati
ya BWANA na mfalme na watu kwamba
watakuwa watu wa BWANA. Akafanya pia
agano kati ya mfalme na watu. 18 [f]Watu
wote wa nchi wakaenda kwenye hekalu
la Baali na kulibomoa. Wakavunjavunja
madhabahu na sanamu, na kumuua Matani
kuhani wa Baali mbele ya hayo madhabahu.

Kisha Yehoyada kuhani akawaweka
walinzi kwenye Hekalu la BWANA.
19 [g]Pamoja naye akawachukua majemadari
wa mamia, Wakari, walinzi na watu wote
wa nchi, nao kwa pamoja wakamteremsha
mfalme kutoka Hekalu la BWANA na kwenda
kwenye jumba la mfalme, wakiingilia
njia ya lango la walinzi. Ndipo mfalme
akachukua nafasi yake kwenye kiti cha
enzi, 20 [h]nao watu wote wa nchi wakafurahi.
Mji ukatulia, kwa sababu Athalia alikuwa
ameuawa kwa upanga nyumbani kwa
mfalme.

21 Yoashi alikuwa na umri wa miaka saba
alipoanza kutawala.

*Yoashi Anakarabati Hekalu*

12 [i]Katika mwaka wa saba wa utawala wa
Yehu, Yoashi alianza kutawala, naye
akatawala huko Yerusalemu miaka arobaini.
Jina la mama yake aliitwa Sibia, kutoka
Beer-Sheba. 2 [j]Yoashi akafanya yaliyo mema
machoni pa BWANA miaka yote ambayo
Yehoyada kuhani alikuwa akimwelekeza.

---

[a]**11:5** 1Nya 9:25
[b]**11:10** 2Sam 8:7
[c]**11:12** Kut 25:16; 1Sam 10:24; Isa 55:12
[d]**11:14** 1Fal 1:39; Mwa 37:29; 2Fal 9:23
[e]**11:17** Kut 24:8; Yer 34:8
[f]**11:18** Kum 12:3; 1Fal 18:40; 2Fal 10:25
[g]**11:19** 2Fal 11:4
[h]**11:20** Mit 11:10
[i]**12:1** 2Fal 11:2
[j]**12:2** Kum 12:25; 2Sam 8:15

[3] [a]Hata hivyo mahali pa juu pa kuabudia
hapakuondolewa. Watu waliendelea kutoa
kafara na kufukiza uvumba huko.
[4] [b]Yoashi akawaambia makuhani,
“Kusanyeni fedha zote ambazo zitaletwa
kama sadaka takatifu kwenye Hekalu la
Bwana, yaani fedha zilizokusanywa kama
kodi, fedha zilizopokelewa kutokana na
nadhiri za watu binafsi, na fedha zilizoletwa
kwa hiari hekaluni. [5] Kila kuhani na apokee
fedha kutoka kwa mmoja wa watunza
hazina, nazo zitumike kukarabati uharibifu
wowote unaoonekana katika Hekalu.”
[6] Lakini ikawa kufikia mwaka wa ishirini
na tatu wa utawala wake Mfalme Yoashi,
makuhani walikuwa bado hawajalikarabati
Hekalu. [7] Kwa hiyo Mfalme Yoashi akamwita
Yehoyada kuhani na makuhani wengine,
akawauliza, “Kwa nini hamtengenezi
uharibifu uliofanyika hekaluni? Msichukue
fedha zaidi kutoka kwa watunza hazina
wenu kwa ajili ya matumizi yenu, lakini
kuanzia sasa ni lazima fedha yote itumike
kwa ajili ya kukarabati Hekalu.” [8] Makuhani
wakakubali kuwa hawatakusanya tena
fedha kutoka kwa watu na kwamba
hawatakarabati Hekalu wenyewe.
[9] [c]Yehoyada kuhani akachukua kisanduku
na akatoboa tundu kwenye kifuniko chake.
Akakiweka kando ya madhabahu upande
wa kulia unapoingia hekaluni mwa Bwana.
Makuhani waliolinda ingilio wakaweka
ndani ya kisanduku fedha zote ambazo
ziliiletwa katika Hekalu la Bwana. [10] [d]Kila
mara walipoona kuwa kuna kiasi kikubwa
cha fedha ndani ya kisanduku, mwandishi
wa mfalme na kuhani mkuu walikuja,
wakazihesabu fedha hizo zilizoletwa katika
Hekalu la Bwana, na kuziweka katika
mifuko. [11] Wakiisha kuthibitisha kiasi cha
hizo fedha, waliwapa watu walioteuliwa
kusimamia kazi katika Hekalu. Kwa fedha
hizo, wakawalipa wale watu waliofanya
kazi katika Hekalu la Bwana: yaani,
maseremala na wajenzi, [12] [e]waashi na
wakata mawe. Walinunua mbao na mawe
ya kuchongwa kwa ajili ya ukarabati wa
Hekalu la Bwana, na kulipia gharama
nyingine zote za kulitengeneza.
[13] [f]Fedha zilizoletwa kwenye Hekalu
hazikutumiwa kutengenezea masinia ya
fedha, mikasi ya kusawazishia tambi,
mabakuli ya kunyunyizia, tarumbeta wala
vyombo vingine vyovyote vya dhahabu
au fedha kwa ajili ya Hekalu la Bwana;
[14] zililipwa kwa wafanyakazi, ambao
walizitumia kwa kukarabati Hekalu.
[15] [g]Wao hawakudai kupewa hesabu ya fedha
kutoka kwa wale waliowapa ili kuwalipa
wafanyakazi, kwa sababu walifanya kwa
uaminifu wote. [16] [h]Fedha zilizopatikana
kutokana na sadaka za hatia na sadaka
za dhambi hazikuletwa katika Hekalu la
Bwana; zilikuwa mali ya makuhani.
[17] [i]Wakati huu Hazaeli mfalme wa
Aramu akapanda kuishambulia Gathi,
akaiteka. Kisha akageuka ili kuishambulia
Yerusalemu. [18] [j]Lakini Yoashi mfalme wa
Yuda akavichukua vyombo vyote vitakatifu
vilivyowekwa wakfu na baba zake, yaani
Yehoshafati, Yehoramu na Ahazia, wafalme
wa Yuda, zawadi ambazo yeye mwenyewe
alikuwa ameziweka wakfu pamoja na
dhahabu yote iliyokutwa katika hazina
za Hekalu la Bwana na katika jumba la
kifalme, akazipeleka kwa Hazaeli mfalme
wa Aramu, ambaye hatimaye aliondoka
Yerusalemu.
[19] Kwa matukio mengine ya utawala
wa Yoashi na yote aliyoyafanya, je,
hayakuandikwa katika kitabu cha
kumbukumbu za wafalme wa Yuda?
[20] [k]Maafisa wake wakafanya shauri baya
dhidi yake, nao wakamuulia Yoashi huko
Beth-Milo, kwenye barabara iteremkayo
kuelekea Sila. [21] Maafisa waliomuua
walikuwa Yozabadi mwana wa Shimeathi,
na Yehozabadi mwana wa Shomeri. Akafa
na akazikwa pamoja na baba zake katika

[a]**12:3** 2Fal 18:4
[b]**12:4** Hes 18:19; Kut 30:12
[c]**12:9** Yer 35:4; Mk 12:41
[d]**12:10** 2Sam 8:17
[e]**12:12** 2Fal 22:5-6
[f]**12:13** 1Fal 7:51
[g]**12:15** 2Fal 22:7; 1Kor 4:2
[h]**12:16** Law 5:14-19
[i]**12:17** 2Fal 8:12
[j]**12:18** 1Fal 15:18; 2Fal 15:20
[k]**12:20** 2Fal 14:5; Amu 9:6

Mji wa Daudi. Naye Amazia mwanawe
akawa mfalme baada yake.

*Yehoahazi Mfalme Wa Israeli*

13 Katika mwaka wa ishirini na tatu wa
utawala wa Yoashi mwana wa Ahazia
mfalme wa Yuda, Yehoahazi mwana wa
Yehu alianza kutawala Israeli katika
Samaria, naye akatawala miaka kumi
na saba. 2 [a]Akafanya maovu machoni pa
BWANA kwa kufuata dhambi za Yeroboamu
mwana wa Nebati, ambazo alikuwa
amesababisha Israeli kuzitenda, na wala
hakuziacha. 3 Kwa hiyo hasira ya BWANA
ikawaka dhidi ya Israeli na kwa muda
mrefu akawaweka chini ya utawala wa
Hazaeli mfalme wa Aramu, na Ben-Hadadi
mwanawe.
4 [b]Ndipo Yehoahazi akamsihi BWANA
rehema, naye BWANA akamsikiliza, kwa
maana aliona jinsi mfalme wa Aramu
alivyokuwa akiwatesa Israeli vikali.
5 [c]BWANA akamtoa mwokozi kwa ajili ya
Israeli, nao wakaokoka kutoka kwenye
mamlaka ya Aramu. Hivyo Waisraeli
wakaishi katika nyumba zao wenyewe
kama ilivyokuwa hapo awali. 6 [d]Lakini
hawakuziacha dhambi za nyumba ya
Yeroboamu, ambazo alisababisha Israeli
kuzitenda, bali wakaendelea kuzitenda.
Nguzo ya Ashera pia iliendelea kusimama
katika Samaria.
7 [e]Hapakubaki kitu chochote katika jeshi
la Yehoahazi isipokuwa wapanda farasi
hamsini, magari kumi ya vita na askari
wa miguu elfu kumi, kwa kuwa mfalme
wa Aramu alikuwa amewaangamiza hao
wengine na kuwafanya kama mavumbi
wakati wa kupura nafaka.
8 Matukio mengine ya utawala wa
Yehoahazi yote aliyoyafanya na mafanikio
yake, je, hayakuandikwa katika kitabu
cha kumbukumbu za wafalme wa Israeli?
9 Yehoahazi akalala pamoja na baba zake,
akazikwa huko Samaria. Naye Yehoashi[f]
mwanawe akawa mfalme baada yake.

*Yehoashi Mfalme Wa Israeli*

10 Katika mwaka wa thelathini na
saba wa utawala wa Yoashi mfalme wa
Yuda, Yehoashi mwana wa Yehoahazi
alianza kutawala Israeli huko Samaria,
naye akatawala miaka kumi na sita.
11 Alifanya maovu machoni pa BWANA,
na hakuacha dhambi yoyote kati ya zile
za Yeroboamu mwana wa Nebati ambazo
alikuwa amesababisha Israeli kuzitenda,
bali aliendelea kuzitenda.
12 [g]Na kwa matukio mengine ya utawala
wa Yehoashi, yote aliyoyafanya na mafanikio
yake, pamoja na vita yake dhidi ya Amazia
mfalme wa Yuda, je, hayakuandikwa katika
kitabu cha kumbukumbu za wafalme wa
Israeli? 13 [h]Yehoashi akalala pamoja na baba
zake, akazikwa Samaria pamoja na wafalme
wa Israeli. Yeroboamu akawa mfalme baada
yake.
14 [i]Wakati huu, Elisha alikuwa anaumwa
na ugonjwa ambao baadaye ulimuua.
Yehoashi mfalme wa Israeli akashuka
kwenda kumwona na kumlilia. Akalia,
“Baba yangu! Baba yangu! Magari ya vita
ya Israeli na wapanda farasi wake!”
15 Elisha akasema, “Leta upinde na
baadhi ya mishale,” naye mfalme akafanya
hivyo. 16 Elisha akamwambia mfalme wa
Israeli, “Shika upinde mikononi mwako.”
Alipokwisha kuichukua, Elisha akaweka
mikono yake juu ya mikono ya mfalme.
17 [j]Elisha akasema, “Fungua dirisha
la mashariki,” naye akalifungua. Elisha
akasema, “Piga mshale!” Naye akapiga
mshale. Elisha akasema, “Mshale wa ushindi
wa BWANA, mshale wa ushindi juu ya
Aramu! Utawaangamiza Waaramu kabisa
huko Afeki.” 18 Kisha akasema, “Chukua
mishale,” naye mfalme akaichukua.
Elisha akamwambia, “Piga ardhi kwa

[a]**13:2** 1Fal 12:26-33
[b]**13:4** Kum 4:29; Hes 10:9
[c]**13:5** Mwa 45:7; Amu 2:18
[d]**13:6** 1Fal 16:33
[e]**13:7** 2Sam 22:43

[f]9 Yehoashi ni namna nyingine ya kutaja jina la Yoashi.
[g]**13:12** 2Fal 14:15
[h]**13:13** 2Fal 14:23; Hos 1:1
[i]**13:14** 2Fal 2:12
[j]**13:17** Yos 8:18; 1Fal 20:26

hiyo mishale.” Akaipiga mara tatu, halafu
akaacha.
19 [a]Mtu wa Mungu akamkasirikia na
akasema, “Ungepiga chini mara tano au sita,
ndipo ungeishinda Aramu na kuiangamiza
kabisa. Lakini sasa utaishinda mara tatu tu.”
20 [b]Elisha akafa, nao wakamzika.
Vikosi vya Wamoabu vilikuwa
vinashambulia nchi kwa vita kila mwaka
wakati wa vuli. 21 [c]Ikawa Waisraeli fulani
walipokuwa wanamzika mtu, ghafula
wakaona kikosi cha washambuliaji, basi
wakaitupa ile maiti ya yule mtu ndani ya
kaburi la Elisha. Wakati ile maiti ilipogusa
mifupa ya Elisha, yule mtu akafufuka na
kusimama kwa miguu yake.
22 [d]Hazaeli mfalme wa Aramu aliwatesa
Israeli wakati wote wa utawala wa
Yehoahazi. 23 [e]Lakini BWANA akawarehemu
na akawahurumia, akaonyesha
kujishughulisha nao kwa sababu ya Agano
lake na Abrahamu, Isaki na Yakobo. Hadi
leo, hajawaangamiza wala kuwafukuza
mbele zake.
24 [f]Hazaeli mfalme wa Shamu akafa,
naye Ben-Hadadi mwanawe akawa mfalme
baada yake. 25 [g]Kisha Yehoashi mwana
wa Yehoahazi akateka tena kutoka kwa
Ben-Hadadi mwana wa Hazaeli ile miji
aliyokuwa ameitwaa kwa vita kutoka kwa
baba yake Yehoahazi. Yehoashi alimshinda
mara tatu, hivyo akaweza kuiteka tena ile
miji ya Waisraeli.

*Amazia Mfalme Wa Yuda*

**(2 Nyakati 25)**

14 Katika mwaka wa pili wa utawala
wa Yehoashi mwana wa Yehoahazi
mfalme wa Israeli, Amazia mwana wa
Yoashi mfalme wa Yuda alianza kutawala.
2 Alikuwa na umri wa miaka ishirini na
mitano alipoanza kutawala, naye akatawala
huko Yerusalemu kwa miaka ishirini na
tisa. Mama yake aliitwa Yehoadani, kutoka
Yerusalemu. 3 Akatenda yaliyo mema
machoni pa BWANA, lakini sio kama Daudi
baba yake alivyokuwa amefanya. Katika
kila kitu alifuata mfano wa Yoashi baba
yake.
4 [h]Hata hivyo mahali pa juu pa kuabudia
hapakuondolewa. Watu waliendelea kutoa
kafara na kufukiza uvumba huko.
5 [i]Baada ya ufalme kuimarika mikononi
mwake, aliwaua maafisa waliomuua mfalme
baba yake. 6 [j]Hata hivyo, hakuwaua wana
wa wale wauaji, sawasawa na ilivyoandikwa
katika Kitabu cha Sheria ya Mose ambako
BWANA aliamuru, “Baba hawatauawa kwa
ajili ya watoto wao, wala watoto kwa ajili
ya baba zao. Kila mmoja atakufa kwa ajili
ya dhambi zake mwenyewe.”
7 [k]Ndiye aliwashinda Waedomu elfu kumi
katika Bonde la Chumvi, na akauteka Sela
katika vita, naye akauita Yoktheeli, jina
ambalo mji huo unalo hadi leo.
8 Kisha Amazia akatuma wajumbe kwa
Yehoashi mwana wa Yehoahazi, mwana wa
Yehu, mfalme wa Israeli, akisema, “Njoo,
tuonane uso kwa uso.”
9 [l]Lakini Yehoashi mfalme wa Israeli
akamjibu Amazia mfalme wa Yuda:
“Mbaruti uliokuwa Lebanoni ulituma
ujumbe kwa mwerezi uliokuwa Lebanoni,
‘Mtoe binti yako aolewe na mwanangu.’
Kisha mnyama wa mwituni aliyekuwa
Lebanoni akaja na kuukanyaga ule mbaruti.
10 [m]Hakika umeishinda Edomu, na sasa
unajivuna. Jisifu katika ushindi wako, lakini
kaa nyumbani kwako! Kwa nini unachokoza
na kujiletea anguko lako mwenyewe na la
Yuda pia?”
11 [n]Hata hivyo, Amazia hakusikia, hivyo
Yehoashi mfalme wa Israeli akashambulia.
Yeye na Amazia mfalme wa Yuda wakakutana
uso kwa uso huko Beth-Shemeshi katika

[a]**13:19** 2Fal 13:25
[b]**13:20** 2Fal 5:2
[c]**13:21** Mt 27:52
[d]**13:22** 1Fal 19:17
[e]**13:23** Kut 2:24; Kum 29:20
[f]**13:24** 2Fal 13:3
[g]**13:25** 2Fal 10:32
[h]**14:4** 2Fal 12:3
[i]**14:5** 2Fal 12:20
[j]**14:6** Yer 31:30; Eze 18:4, 20
[k]**14:7** 2Sam 8:13; Amu 1:36
[l]**14:9** Amu 9:8-15
[m]**14:10** 2Nya 26:16
[n]**14:11** Yos 15:10

Yuda. 12 [a]Yuda ikashindwa na Israeli, na
kila mtu akakimbilia nyumbani kwake.
13 [b]Yehoashi mfalme wa Israeli akamteka
Amazia mfalme wa Yuda, mwana wa Yoashi,
mwana wa Ahazia, huko Beth-Shemeshi.
Kisha Yehoashi akaenda Yerusalemu na
kuubomoa ukuta wa Yerusalemu kuanzia
Lango la Efraimu hadi Lango la Pembeni,
sehemu yenye urefu wa kama dhiraa 400.[c]
14 Akachukua dhahabu yote na fedha na
vyombo vyote vilivyopatikana ndani ya
Hekalu la Bwana na katika hazina zote
za jumba la mfalme. Akachukua pia mateka
na akarudi Samaria.

15 [d]Matukio mengine ya utawala wa
Yehoashi, aliyoyafanya na mafanikio yake,
pamoja na vita vyake dhidi ya Amazia
mfalme wa Yuda, je, hayakuandikwa katika
kitabu cha kumbukumbu za wafalme wa
Israeli? 16 Yehoashi akalala pamoja na baba
zake, akazikwa Samaria pamoja na wafalme
wa Israeli, naye Yeroboamu mwanawe
akawa mfalme baada yake.

17 Amazia mwana wa Yoashi mfalme wa
Yuda aliishi miaka kumi na mitano baada
ya kifo cha Yehoashi mwana wa Yehoahazi
mfalme wa Israeli. 18 Matukio mengine ya
utawala wa Amazia, je, hayakuandikwa
katika kitabu cha kumbukumbu za wafalme
wa Yuda?

19 [e]Wakafanya shauri baya dhidi ya Amazia
huko Yerusalemu, naye akakimbilia Lakishi,
lakini wakawatuma watu wamfuatilie
huko Lakishi, nao wakamuulia huko.
20 Akarudishwa kwa farasi na akazikwa
huko Yerusalemu pamoja na baba zake
katika Mji wa Daudi.

21 [f]Kisha watu wote wa Yuda
wakamchukua Azaria[g] aliyekuwa na umri
wa miaka kumi na sita, na kumfanya
mfalme mahali pa baba yake Amazia.
22 Ndiye aliijenga tena Elathi na kuirudisha
kwa Yuda baada ya Amazia kulala pamoja
na baba zake.

### *Yeroboamu Wa Pili Mfalme Wa Israeli*

23 [h]Katika mwaka wa kumi na tano wa
utawala wa Amazia mwana wa Yoashi
mfalme wa Yuda, Yeroboamu mwana
wa Yehoashi mfalme wa Israeli alianza
kutawala huko Samaria, naye akatawala
kwa miaka arobaini na mmoja. 24 Akafanya
maovu machoni pa Bwana, na hakuacha
dhambi hata moja ya Yeroboamu mwana
wa Nebati, ambazo alikuwa amesababisha
Israeli kuzitenda. 25 [i]Ndiye alirudishia
mipaka ya Israeli kuanzia Lebo-Hamathi
hadi Bahari ya Araba, sawasawa na neno
la Bwana, Mungu wa Israeli, lililosemwa
kupitia mtumishi wake Yona mwana wa
Amitai, nabii kutoka Gath-Heferi.

26 [j]Bwana alikuwa ameona jinsi kila
mmoja katika Israeli, awe mtumwa au
aliye huru, alivyoteseka kwa uchungu;
hapakuwepo na yeyote wa kuwasaidia.
27 [k]Kwa kuwa Bwana alikuwa hajasema
kuwa atafuta jina la Israeli chini ya mbingu,
akawaokoa kwa mkono wa Yeroboamu
mwana wa Yehoashi.

28 [l]Kwa matukio mengine ya utawala
wa Yeroboamu, yote aliyoyafanya na
mafanikio yake ya kijeshi, ikiwa ni
pamoja na jinsi alivyorudisha Dameski na
Hamathi kwa Israeli, ambayo ilikuwa mali
ya Yuda, je, hayakuandikwa katika kitabu
cha kumbukumbu za wafalme wa Israeli?
29 Yeroboamu akalala pamoja na baba zake,
wafalme wa Israeli. Naye Zekaria mwanawe
akawa mfalme baada yake.

### *Azaria Mfalme Wa Yuda*

**(2 Nyakati 26)**

15 [m]Katika mwaka wa ishirini na saba wa
utawala wa Yeroboamu mfalme wa
Israeli, Azaria mwana wa Amazia mfalme
wa Yuda alianza kutawala. 2 Alikuwa na

---

[a]**14:12** 1Fal 22:36
[b]**14:13** Neh 8:16; Yer 31:38; Zek 14:10
[c]13 Dhiraa 400 ni sawa na mita 180.
[d]**14:15** 2Fal 13:12
[e]**14:19** 2Fal 12:20; Yos 10:3
[f]**14:21** 2Nya 26:23; Amo 1:1
[g]21 Azaria pia aliitwa Uzia.
[h]**14:23** 2Fal 13:13; 1Nya 5:17
[i]**14:25** Hes 13:21; Mt 12:39
[j]**14:26** Kum 32:36; 2Fal 13:4; Mao 1:7
[k]**14:27** Kum 29:20; Amu 6:14
[l]**14:28** 2Sam 8:5; 1Fal 15:31
[m]**15:1** 2Fal 14:21

umri wa miaka kumi na sita alipoanza
kutawala, naye akatawala huko Yerusalemu
kwa miaka hamsini na miwili. Mama yake
aliitwa Yekolia wa Yerusalemu. 3 Akatenda
yaliyo mema machoni pa BWANA, kama
Amazia baba yake alivyofanya. 4 Hata
hivyo, mahali pa juu pa kuabudia
hapakuondolewa. Watu waliendelea kutoa
kafara na kufukiza uvumba huko.
5 [a]BWANA akampiga mfalme kwa ukoma
mpaka siku aliyokufa, naye aliishi katika
nyumba iliyotengwa peke yake. Yothamu
mwana wa mfalme akawa msimamizi wa
jumba la mfalme, na akawatawala watu
wa nchi.
6 Matukio mengine ya utawala wa Azaria
na yote aliyoyafanya, je, hayakuandikwa
katika kitabu cha kumbukumbu za wafalme
wa Yuda? 7 [b]Azaria akalala pamoja na baba
zake, naye akazikwa karibu nao katika Mji
wa Daudi, na Yothamu mwanawe akawa
mfalme baada yake.

*Zekaria Mfalme Wa Israeli*

8 Katika mwaka wa thelathini na nane
wa utawala wa Azaria mfalme wa Yuda,
Zekaria mwana wa Yeroboamu akawa
mfalme wa Israeli katika Samaria, naye
akatawala miezi sita. 9 Akafanya maovu
machoni pa BWANA, kama baba zake
walivyofanya. Hakuziacha dhambi za
Yeroboamu mwana wa Nebati ambazo
alisababisha Israeli kuzitenda.
10 [c]Shalumu mwana wa Yabeshi
akafanya shauri baya dhidi ya Zekaria.
Akamshambulia mbele ya watu, akamuua
na kuingia mahali pake kuwa mfalme.
11 Matukio mengine ya utawala wa
Zekaria yameandikwa kwenye kitabu cha
kumbukumbu za wafalme wa Israeli. 12 [d]Kwa
hiyo neno la BWANA lililonenwa kwa Yehu
likatimia, kwamba, "Wazao wako wataketi
juu ya kiti cha enzi cha Israeli hadi kizazi
cha nne."

[a]**15:5** Law 13:46; Mwa 41:40
[b]**15:7** Isa 6:1
[c]**15:10** 2Fal 12:20
[d]**15:12** 2Fal 10:30

*Shalumu Mfalme Wa Israeli*

13 Shalumu mwana wa Yabeshi akawa
mfalme katika mwaka wa thelathini na tisa
wa Uzia mfalme wa Yuda, naye akatawala
katika Samaria kwa mwezi mmoja. 14 [e]Kisha
Menahemu mwana wa Gadi akaenda kutoka
Tirsa mpaka Samaria. Akamshambulia
Shalumu mwana wa Yabeshi huko Samaria,
akamuua na kuingia mahali pake kuwa
mfalme.
15 Matukio mengine ya utawala wa
Shalumu, na mauaji aliyoyafanya,
yameandikwa katika kitabu cha
kumbukumbu za wafalme wa Israeli.
16 [f]Wakati ule, akianzia Tirsa, Menahemu
alishambulia Tifsa na kila mtu ndani yake,
na wale waliokuwa maeneo jirani, kwa
sababu walikataa kufungua malango yao.
Akaiangamiza Tifsa yote, na kuwapasua
matumbo wanawake wote wenye mimba.

*Menahemu Mfalme Wa Israeli*

17 Katika mwaka wa thelathini na tisa
wa utawala wa Azaria mfalme wa Yuda,
Menahemu mwana wa Gadi akawa mfalme
wa Israeli, akatawala huko Samaria kwa
miaka kumi. 18 Akatenda maovu machoni
pa BWANA. Katika wakati wa utawala wake
wote, hakuziacha dhambi za Yeroboamu
mwana wa Nebati ambazo alisababisha
Israeli kuzitenda.
19 [g]Kisha Pulu mfalme wa Ashuru
akaishambulia Israeli. Menahemu mfalme
wa Israeli akampa talanta elfu moja za
fedha[h] ili amsaidie na kumwezesha katika
utawala wake. 20 [i]Menahemu akatoza fedha
hizi kwa nguvu kutoka kwa Israeli. Kila mtu
tajiri alilazimika kuchanga shekeli hamsini
za fedha[j] ambazo alipewa mfalme wa
Ashuru. Basi mfalme wa Ashuru akajiondoa
na hakuendelea kuikalia nchi.
21 Matukio mengine ya utawala wa

[e]**15:14** 1Fal 15:33; 2Fal 12:20
[f]**15:16** 2Fal 8:12; Hos 13:16
[g]**15:19** 1Nya 5:6, 26
[h]19 Talanta 1,000 za fedha ni sawa na tani 34.
[i]**15:20** 2Fal 12:18
[j]20 Shekeli 50 za fedha ni sawa na gramu 600.

Menahemu na yote aliyoyafanya, je,
hayakuandikwa katika kitabu cha
kumbukumbu za wafalme wa Israeli?
22 Menahemu akalala pamoja na baba zake.
Naye Pekahia mwanawe akawa mfalme
baada yake.

*Pekahia Mfalme Wa Israeli*

23 Katika mwaka wa hamsini wa utawala
wa Azaria mfalme wa Yuda, Pekahia
mwana wa Menahemu akawa mfalme
wa Israeli huko Samaria, akatawala
miaka miwili. 24 Pekahia akafanya uovu
machoni pa Bwana. Hakuziacha dhambi
za Yeroboamu mwana wa Nebati, ambazo
alisababisha Israeli kuzitenda. 25 [a]Mmoja
wa maafisa wake wakuu, Peka mwana
wa Remalia, akafanya shauri baya dhidi
yake. Akachukua watu hamsini wa Gileadi
pamoja naye, akamuua Pekahia, pamoja na
Argobu na Aria, katika ngome ya jumba
la kifalme huko Samaria. Kwa hiyo Peka
akamuua Pekahia, naye akaingia mahali
pake kuwa mfalme.
26 Matukio mengine ya utawala wa
Pekahia na yote aliyoyafanya yameandikwa
katika kitabu cha kumbukumbu za wafalme
wa Israeli.

*Peka Mfalme Wa Israeli*

27 [b]Katika mwaka wa hamsini na mbili
wa utawala wa Azaria mfalme wa Yuda,
Peka mwana wa Remalia akawa mfalme wa
Israeli huko Samaria, naye alitawala miaka
ishirini. 28 Akafanya maovu machoni pa
Bwana. Hakuziacha dhambi za Yeroboamu
mwana wa Nebati, ambazo alisababisha
Israeli kuzitenda.
29 [c]Wakati wa utawala wa Peka mfalme wa
Israeli, Tiglath-Pileseri mfalme wa Ashuru
alikuja na kuteka Iyoni, Abel-Beth-Maaka,
Yanoa, Kedeshi na Hazori. Akateka miji ya
Gileadi na Galilaya, pamoja na nchi yote
ya Naftali, na kuwahamishia watu wote
Ashuru. 30 [d]Kisha Hoshea mwana wa Ela
akafanya shauri baya dhidi ya Peka mwana
wa Remalia. Akamshambulia na kumuua,
kisha akaingia mahali pake kuwa mfalme
katika mwaka wa ishirini wa Yothamu
mwana wa Uzia.
31 Matukio mengine ya utawala wa Peka
na yote aliyoyafanya, je, hayakuandikwa
katika kitabu cha kumbukumbu za wafalme
wa Israeli?

*Yothamu Mfalme Wa Yuda*

**(2 Nyakati 27)**

32 [e]Katika mwaka wa pili wa utawala wa
Peka mwana wa Remalia mfalme wa Israeli,
Yothamu mwana wa Uzia mfalme wa Yuda
alianza kutawala. 33 Alikuwa na miaka
ishirini na mitano alipoanza kutawala,
naye akatawala huko Yerusalemu miaka
kumi na sita. Mama yake aliitwa Yerusha
binti Sadoki. 34 [f]Akafanya yaliyo mema
machoni pa Bwana, kama Uzia baba yake
alivyokuwa amefanya. 35 Hata hivyo, mahali
pa juu pa kuabudia hapakuondolewa. Watu
waliendelea kutoa kafara na kufukiza
uvumba huko. Yothamu akajenga upya
Lango la Juu la Hekalu la Bwana.
36 Matukio mengine ya utawala
wa Yothamu na yale aliyoyafanya,
je, hayakuandikwa katika kitabu cha
kumbukumbu za wafalme wa Yuda?
37 [g](Katika siku hizo, Bwana akaanza
kuwatuma Resini mfalme wa Aramu na
Peka mwana wa Remalia dhidi ya Yuda.)
38 Yothamu akalala na baba zake, akazikwa
pamoja nao katika Mji wa Daudi, mji wa
baba zake. Naye Ahazi mwanawe akawa
mfalme baada yake.

*Ahazi Mfalme Wa Yuda*

**(2 Nyakati 28)**

16 [h]Katika mwaka wa kumi na saba wa
utawala wa Peka mwana wa Remalia,
Ahazi mwana wa Yothamu mfalme wa
Yuda alianza kutawala. 2 Ahazi alikuwa
na miaka ishirini alipoanza kutawala,
akatawala huko Yerusalemu kwa miaka

[a]**15:25** 2Nya 28:6; Isa 7:1
[b]**15:27** 2Nya 28:6; Isa 7:4
[c]**15:29** 1Nya 5:26; Yer 50:17; Isa 14:6, 17
[d]**15:30** 2Fal 17:1
[e]**15:32** 1Nya 5:17
[f]**15:34** 1Fal 14:8
[g]**15:37** 2Fal 16:5
[h]**16:1** Isa 1:1; Hos 1:1

kumi na sita. Tofauti na Daudi baba yake,
hakufanya yaliyo mema machoni pa Bwana,
Mungu wake. 3 [a]Akaenenda katika njia
za wafalme wa Israeli, na hata akamtoa
mwanawe kafara katika moto, akifuata njia
za machukizo za mataifa ambayo BWANA
alikuwa ameyafukuza mbele ya Waisraeli.
4 [b]Akatoa kafara na kufukiza uvumba katika
mahali pa juu pa kuabudia miungu, juu ya
vilima, na chini ya kila mti uliotanda.

5 [c]Kisha Resini mfalme wa Aramu na
Peka mwana wa Remalia mfalme wa
Israeli wakaondoka kwenda kupigana
dhidi ya Yerusalemu na kumzunguka
Ahazi kwa jeshi, lakini hawakuweza
kumshinda. 6 [d]Wakati ule, Resini mfalme
wa Aramu akaurudisha Elathi kwa Aramu
kwa kuwafukuza watu wa Yuda. Kisha
Waedomu wakahamia Elathi, nao wanaishi
huko mpaka leo.

7 [e]Ahazi akatuma wajumbe kumwambia
Tiglath-Pileseri mfalme wa Ashuru kwamba,
"Mimi ni mtumishi na mtumwa wako. Njoo
na uniokoe kutoka mkononi mwa mfalme
wa Aramu na wa mfalme wa Israeli,
ambao wananishambulia." 8 [f]Naye Ahazi
akachukua fedha na dhahabu zilizopatikana
ndani ya Hekalu la BWANA na katika hazina
ya jumba la mfalme, na kuzituma kama
zawadi kwa mfalme wa Ashuru. 9 [g]Mfalme
wa Ashuru akamwitikia kwa kushambulia
Dameski na kuiteka. Akawahamishia
wenyeji wake huko Kiri, na kumuua Resini.

10 [h]Kisha Mfalme Ahazi akaenda Dameski
kukutana na Tiglath-Pileseri wa Ashuru.
Akaona madhabahu huko Dameski, naye
akamtumia Uria kuhani mchoro wa hayo
madhabahu, pamoja na maelezo ya mpango
kamili wa ujenzi wake. 11 Kwa hiyo Uria
kuhani akajenga madhabahu kulingana
na mipango yote ambayo Mfalme Ahazi
alikuwa ameituma kutoka Dameski, na
akamaliza ujenzi kabla ya Mfalme Ahazi
kurudi. 12 [i]Mfalme aliporudi kutoka Dameski
na kuona hayo madhabahu, akayasogelea
na kutoa sadaka juu yake. 13 Akatoa
sadaka yake ya kuteketezwa na sadaka ya
nafaka, akamimina sadaka ya kinywaji na
kunyunyizia damu ya sadaka zake za amani
juu ya hayo madhabahu. 14 [j]Mfalme Ahazi
akayaondoa madhabahu ya zamani ya shaba
kutoka hapo mbele ya Hekalu la BWANA,
yaliyokuwa yamesimama kati ya ingilio la
Hekalu na hayo madhabahu mapya, naye
akayaweka upande wa kaskazini mwa hayo
madhabahu mapya.

15 [k]Ndipo Mfalme Ahazi akatoa amri
zifuatazo kwa Uria kuhani: "Juu ya hayo
madhabahu kubwa mapya, toa sadaka
ya asubuhi ya kuteketezwa na sadaka
ya jioni ya nafaka, sadaka ya mfalme ya
kuteketezwa pamoja na sadaka yake ya
nafaka, sadaka ya kuteketezwa ya watu
wote wa nchi, pamoja na sadaka yao
ya nafaka na sadaka yao ya kinywaji.
Unyunyize juu ya hayo madhabahu damu
yote ya sadaka za kuteketezwa na dhabihu.
Lakini mimi nitatumia hayo madhabahu
ya zamani ya shaba kwa ajili ya kutafuta
uongozi." 16 Naye Uria kuhani akafanya
kama Mfalme Ahazi alivyoagiza.

17 [l]Mfalme Ahazi akaondoa mbao za
pembeni na kuondoa masinia kwenye vile
vishikilio vilivyohamishika. Akaondoa ile
Bahari kutoka kwenye mafahali wa shaba
walioishikilia, na kuiweka kwenye kitako
cha jiwe. 18 [m]Kwa heshima ya mfalme wa
Ashuru, akaliondoa pia pazia la Sabato
lililokuwa limewekwa ndani ya Hekalu,
na akaondoa ile njia ya kifalme ya kuingia
kwenye Hekalu la BWANA.

19 Matukio mengine ya utawala wa Ahazi
na yale aliyoyafanya, je hayakuandikwa
katika kitabu cha kumbukumbu za wafalme
wa Yuda? 20 [n]Ahazi akalala na baba zake,
naye akazikwa pamoja nao katika Mji wa

[a]**16:3** Law 18:21; Kum 9:4
[b]**16:4** Kum 12:2; Eze 6:13
[c]**16:5** 2Fal 15:37
[d]**16:6** Isa 9:12; 1Fal 9:26
[e]**16:7** 2Fal 15:29; Hos 10:6
[f]**16:8** 2Fal 12:18; 12:18
[g]**16:9** Mwa 14:15; Amo 1:5
[h]**16:10** Isa 6:2
[i]**16:12** 2Nya 26:16
[j]**16:14** Kut 40:6; 1Fal 8:64
[k]**16:15** Kut 29:38-41
[l]**16:17** 1Fal 7:27
[m]**16:18** Eze 16:28
[n]**16:20** Isa 14:28

Daudi. Naye Hezekia mwanawe akawa
mfalme baada yake.

*Hoshea, Mfalme Wa Mwisho Katika Israeli*

17 [a]Katika mwaka wa kumi na mbili wa
utawala wa Ahazi mfalme wa Yuda,
Hoshea mwana wa Ela akawa mfalme wa
Israeli katika Samaria, akatawala kwa
miaka tisa. 2 [b]Akafanya maovu machoni pa
BWANA, lakini si kama wafalme wengine
wa Israeli waliomtangulia.
3 [c]Mfalme Shalmanesa wa Ashuru
akainuka dhidi ya Mfalme Hoshea, ambaye
hapo mbeleni alikuwa mtumwa wake na
kumlipa ushuru. 4 [d]Lakini mfalme wa
Ashuru akagundua kuwa Hoshea alikuwa
msaliti, kwa kuwa alikuwa ametuma
wajumbe kwa So mfalme wa Misri, naye
hakuendelea kulipa ushuru kwa mfalme wa
Ashuru tena kama alivyokuwa anafanya kila
mwaka. Kwa hiyo Shalmanesa akamkamata
na kumtia gerezani. 5 Mfalme wa Ashuru
akaishambulia nchi yote, akapigana dhidi
ya Samaria na kuizunguka kwa majeshi
miaka mitatu. 6 [e]Katika mwaka wa tisa
wa Hoshea, mfalme wa Ashuru akaiteka
Samaria na kuwahamishia Waisraeli huko
Ashuru. Akawaweka huko Hala, na Gozani
karibu na Mto Habori, na katika miji ya
Wamedi.

*Israeli Inakwenda Uhamishoni Kwa Sababu Ya Dhambi*

7 [f]Yote haya yalitokea kwa sababu
Waisraeli walikuwa wametenda dhambi
dhidi ya BWANA Mungu wao, ambaye
alikuwa amewapandisha kutoka Misri
akiwatoa chini ya utawala wa nguvu wa
Farao mfalme wa Misri. Waliabudu miungu
mingine 8 [g]na kufuata desturi za mataifa
ambayo BWANA alikuwa ameyafukuza
mbele yao, pamoja na desturi ambazo
wafalme wa Israeli walizileta. 9 [h]Waisraeli
wakafanya vitu kwa siri dhidi ya BWANA
Mungu wao, ambavyo havikuwa sawa.
Kuanzia kwenye mnara wa ulinzi hadi
kwenye mji wenye maboma walijijengea
wenyewe mahali pa juu pa kuabudia
miungu katika miji yao yote. 10 [i]Wakaweka
mawe ya kuabudiwa na nguzo za Ashera
juu ya kila kilima kirefu na chini ya kila
mti uliotanda. 11 Wakafukiza uvumba kila
mahali palipoinuka, kama yalivyofanya
yale mataifa ambayo BWANA alikuwa
ameyafukuza mbele yao. Wakafanya
mambo maovu ambayo yalimghadhibisha
BWANA. 12 [j]Wakaabudu sanamu, ingawa
BWANA alikuwa amesema, "Msifanye
mambo haya." 13 [k]BWANA akawaonya Israeli
na Yuda kupitia kwa manabii na waonaji
wake wote: "Acheni njia zenu mbaya.
Shikeni amri na maagizo yangu, kufuatana
na sheria yangu yote niliyowaagiza baba
zenu kuitii ambayo niliileta kwenu kupitia
kwa watumishi wangu manabii."
14 [l]Lakini hawakusikiliza, walikuwa na
shingo ngumu kama baba zao, ambao
hawakumtegemea BWANA Mungu wao.
15 [m]Walizikataa amri zake, na agano
alilokuwa amelifanya na baba zao, na
maonyo aliyokuwa amewapa. Wakafuata
sanamu zisizofaa, nao wenyewe
wakawa hawafai. Wakayaiga mataifa
yaliyowazunguka, ingawa BWANA alikuwa
amewaonya akiwaambia, "Msifanye kama
wanavyofanya," nao wakafanya mambo
ambayo BWANA alikuwa amewakataza
wasifanye.
16 [n]Wakayaacha maagizo yote ya BWANA
Mungu wao na kujitengenezea sanamu
mbili, walizozisubu katika sura ya ndama
na nguzo ya Ashera. Wakasujudia mianga
yote ya angani, na wakamtumikia Baali.
17 [o]Wakawatoa kafara wana wao na mabinti

[a]**17:1** 2Fal 15:30
[b]**17:2** Kum 4:25
[c]**17:3** Hos 10:14; Amu 3:15
[d]**17:4** Za 146:3; Hos 13:10
[e]**17:6** 2Fal 15:29; Isa 10:9
[f]**17:7** Yos 7:11; Kut 14:15-31
[g]**17:8** Law 18:3; Kum 9:4
[h]**17:9** 2Fal 18:8
[i]**17:10** Kut 34:13; Mik 5:14
[j]**17:12** Kut 20:4
[k]**17:13** 1Sam 9:9; Yer 18:11; Zek 1:4
[l]**17:14** Kut 32:9; Mdo 7:15
[m]**17:15** Law 26:11; Kum 32:21
[n]**17:16** Kut 32:4; Yer 2:5
[o]**17:17** Kum 18:10-12; Rum 7:14

zao katika moto. Wakafanya uaguzi na
uchawi, nao wakajiuza wenyewe katika
kutenda uovu machoni pa Bwana,
wakamghadhibisha.
18 Basi Bwana akawakasirikia sana
Israeli na kuwaondoa kwenye uwepo wake.
Ni kabila la Yuda tu lililobaki; 19 na hata
hivyo nao Yuda hawakuzishika amri za
Bwana Mungu wao. Wakafuata desturi
ambazo Israeli walikuwa wamezianzisha.
20 [a]Kwa hiyo Bwana aliwakataa watu wote
wa Israeli; akawatesa na kuwaachia katika
mikono ya wateka nyara hadi alipowaondoa
kutoka kwenye uwepo wake.
21 [b]Alipokwisha kuwatenga Israeli
mbali na nyumba ya Daudi, wakamfanya
Yeroboamu mwana wa Nebati kuwa
mfalme wao. Yeroboamu akawashawishi
Israeli waache kumfuata Bwana na
akawasababisha kutenda dhambi kuu.
22 Nao Israeli wakadumu katika dhambi
zote za Yeroboamu mwana wa Nebati,
nao hawakuziacha 23 [c]hadi Bwana
alipowaondoa kutoka kwenye uwepo wake,
kama vile alivyokuwa ameonya kupitia
watumishi wake wote manabii. Hivyo watu
wa Israeli wakaondolewa kutoka nchi yao
kwenda uhamishoni Ashuru, nao wako
huko mpaka sasa.

### *Samaria Inakaliwa Tena*

24 [d]Mfalme wa Ashuru akawaleta watu
kutoka Babeli, Kutha, Ava, Hamathi
na Sefarvaimu na kuwaweka katika
miji ya Samaria badala ya Waisraeli.
Wakaimiliki Samaria na kuishi katika miji
yake. 25 [e]Wakati walianza kuishi humo,
hawakumwabudu Bwana, kwa hiyo
akatuma simba miongoni mwao, wakawaua
baadhi ya watu. 26 Habari ikapelekwa
kwa mfalme wa Ashuru, kusema: “Watu
uliowahamisha na kuwaweka katika miji ya
Samaria hawajui kile Mungu wa nchi hiyo
anachokitaka. Ametuma simba miongoni
mwao, ambao wanawaua, kwa sababu watu
hawajui anachokitaka.”
27 Ndipo mfalme wa Ashuru akaamuru
hivi: “Mtwae mmoja wa makuhani
uliowachukua mateka kutoka Samaria ili
arudi kuishi humo na awafundishe watu kile
ambacho Mungu wa nchi anataka.” 28 Basi
mmoja wa makuhani ambaye alikuwa
amepelekwa uhamishoni kutoka Samaria
akaja kuishi Betheli na kuwafundisha jinsi
ya kumwabudu Bwana.
29 [f]Hata hivyo, kila kikundi cha taifa
lililoletwa Samaria kilitengeneza miungu
yao wenyewe katika miji kadhaa mahali
walipoishi, nao wakaiweka mahali pa
ibada za miungu ambapo watu wa Samaria
walikuwa wametengeneza katika mahali pa
juu. 30 Watu kutoka Babeli wakamtengeneza
Sukoth-Benothi kuwa mungu wao, watu
kutoka Kutha wakamtengeneza Nergali,
na watu kutoka Hamathi wakamtengeneza
Ashima; 31 [g]Waavi wakatengeneza Nibhazi
na Tartaki, nao Wasefarvi wakachoma
watoto wao kama kafara kwa Adrameleki
na Anameleki, miungu ya Sefarvaimu.
32 [h]Walimwabudu Bwana, lakini pia
waliteua aina zote za watu wao ili
kuwawakilisha kama makuhani katika
mahali pa kuabudia miungu kwenye
mahali pa juu pa ibada. 33 Walimwabudu
Bwana, lakini pia waliitumikia miungu yao
kulingana na desturi za mataifa walikotoka.
34 [i]Mpaka leo wanashikilia desturi zao
za zamani. Hawamwabudu Bwana wala
kuzishika hukumu na maagizo, sheria
na amri ambazo Bwana aliwapa uzao
wa Yakobo, ambaye alimwita Israeli.
35 [j]Wakati Bwana alipofanya Agano na
Waisraeli, aliwaamuru akisema: “Msiiabudu
miungu mingine yoyote wala kuisujudia,
wala kuitumikia wala kuitolea dhabihu.
36 [k]Bali imewapasa kumwabudu Bwana
aliyewapandisha kutoka Misri kwa
uwezo wake mkuu na kwa mkono wake

[a]**17:20** 2Fal 17:6
[b]**17:21** 1Sam 15:27; 1Fal 12:20
[c]**17:23** Eze 39:23-24; Amu 6:8
[d]**17:24** 2Fal 18:34; Amo 6:2
[e]**17:25** Mwa 37:20; Yer 50:17
[f]**17:29** Yer 2:28; Mik 4:5
[g]**17:31** 2Fal 17:24
[h]**17:32** 1Fal 12:31
[i]**17:34** Mwa 17:5; 1Fal 18:31
[j]**17:35** Kut 20:3
[k]**17:36** Kum 3:20; Za 136:12

ulionyooshwa. Kwake yeye mtasujudu na
kwake yeye mtatoa dhabihu. 37 [a]Imewapasa
daima kuwa waangalifu kutunza hukumu
na maagizo, sheria na amri alizowaandikia.
Msiabudu miungu mingine. 38 [b]Msisahau
agano nililofanya nanyi, wala msiabudu
miungu mingine. 39 Bali, mtamwabudu
Bwana Mungu wenu, kwani yeye ndiye
atakayewakomboa kutoka mikononi mwa
adui zenu wote."

40 Hata hivyo hawakusikiliza, lakini
waliendelea na desturi zao za awali.
41 [c]Hata wakati watu hawa walipokuwa
wanamwabudu Bwana, walikuwa bado
wakitumikia sanamu zao. Mpaka leo watoto
wao na watoto wa watoto wao wanaendelea
kufanya kama baba zao walivyofanya.

*Hezekia Mfalme Wa Yuda*

**(2 Nyakati 29:1–31:21)**

18 [d]Katika mwaka wa tatu wa utawala
wa Hoshea mwana wa Ela mfalme wa
Israeli, Hezekia mwana wa Ahazi mfalme
wa Yuda alianza kutawala. 2 [e]Alikuwa
na umri wa miaka ishirini na mitano
alipoanza kutawala, naye akatawala huko
Yerusalemu kwa miaka ishirini na tisa.
Mama yake aliitwa Abiya binti Zekaria.
3 [f]Akafanya yaliyo mema machoni pa
Bwana, kama Daudi baba yake alivyofanya.
4 [g]Akapaondoa mahali pa juu pa kuabudia
miungu, akazivunja sanamu, akakatakata
nguzo za Ashera. Akavunja vipande vipande
ile nyoka ya shaba Mose aliyotengeneza,
kwa kuwa hadi siku hizo wana wa Israeli
walikuwa wanaifukizia uvumba (ilikuwa
ikiitwa Nehushtani[h]).

5 [i]Hezekia aliweka tumaini lake kwa
Bwana, Mungu wa Israeli. Hapakuwepo
na mfalme mwingine wa kufanana naye
miongoni mwa wafalme wa Yuda, kabla
yake au baada yake. 6 [j]Alishikamana na
Bwana kwa bidii wala hakuacha kumfuata;
alishika amri ambazo Bwana alikuwa
amempa Mose. 7 [k]Naye Bwana alikuwa
pamoja naye, akafanikiwa katika kila
alichokifanya. Aliasi dhidi ya mfalme wa
Ashuru, wala hakumtumikia. 8 [l]Kuanzia
mnara wa ulinzi hadi kwenye mji wenye
ngome, aliwashinda Wafilisti, hadi kufikia
Gaza na himaya yake yote.

9 [m]Mwaka wa nne wa Mfalme Hezekia,
ambao ulikuwa mwaka wa saba wa
Hoshea mwana wa Ela kutawala Israeli,
Shalmanesa mfalme wa Ashuru alikwenda
kuishambulia Samaria na kuuzunguka
kwa majeshi. 10 Baada ya miaka mitatu
Waashuru wakautwaa. Kwa hiyo Samaria
ulitekwa katika mwaka wa sita wa utawala
wa Mfalme Hezekia, ambao ulikuwa
mwaka wa tisa wa utawala wa Hoshea
mfalme wa Israeli. 11 [n]Mfalme wa Ashuru
akawahamishia Waisraeli huko Ashuru
na akawaweka Hala, na Gozani karibu na
Mto Habori, na katika miji ya Wamedi.
12 [o]Hili lilitokea kwa sababu hawakumtii
Bwana Mungu wao, lakini walikuwa
wamevunja agano lake, yale yote ambayo
Mose mtumishi wa Bwana aliwaamuru.
Hawakuzisikiliza amri wala kuzitimiza.

13 Katika mwaka wa kumi na nne wa
utawala wa Mfalme Hezekia, Senakeribu
mfalme wa Ashuru akaishambulia miji yote
ya Yuda yenye ngome na kuiteka. 14 [p]Basi
Hezekia mfalme wa Yuda akamtumia
ujumbe mfalme wa Ashuru huko Lakishi
akisema: "Nimefanya makosa. Ondoka
katika nchi yangu, nami nitakulipa
chochote unachokitaka kwangu." Mfalme
wa Ashuru akamtoza Hezekia mfalme wa
Yuda talanta 300[q] za fedha, na talanta

[a]**17:37** Kum 5:32; Law 19:37
[b]**17:38** Kum 6:12
[c]**17:41** 1Fal 18:21; Mt 6:24
[d]**18:1** Hos 1:1; Mik 1:1
[e]**18:2** Isa 38:5
[f]**18:3** 1Fal 14:8; Isa 38:5
[g]**18:4** 2Nya 31:1; Hes 21:9
[h]4 Nehushtani maana yake Kipande cha shaba.
[i]**18:5** 2Fal 19:10; Mit 3:26
[j]**18:6** Kum 6:18
[k]**18:7** Mwa 39:3; Ezr 4:19
[l]**18:8** 2Fal 17:9
[m]**18:9** Isa 1:1
[n]**18:11** Isa 37:12; Eze 16:39
[o]**18:12** Dan 9:6, 10; 1Fal 9:6
[p]**18:14** 2Fal 19:8; Isa 24:5
[q]14 Talanta 300 za fedha ni sawa na tani 10.

thelathini[a] za dhahabu. 15 [b]Basi Hezekia
akampa fedha yote iliyopatikana ndani
ya Hekalu la BWANA na katika hazina ya
jumba la mfalme.
16 Wakati huu Hezekia mfalme wa
Yuda akabandua dhahabu yote iliyokuwa
imefunika milango na miimo ya Hekalu la
BWANA, akampa mfalme wa Ashuru.

*Senakeribu Anaitishia Yerusalemu*

**(2 Nyakati 32:1-19; Isaya 36:1-22)**

17 [c]Mfalme wa Ashuru akamtuma
jemadari wake mkuu, na afisa wake mkuu,
na jemadari wa jeshi, pamoja na jeshi kubwa
kutoka Lakishi hadi kwa Mfalme Hezekia
huko Yerusalemu. Wakaja Yerusalemu na
kusimama kwenye mfereji wa Bwawa la
Juu, lililojengwa katika barabara iendayo
kwenye Uwanja wa Dobi. 18 [d]Wakaagiza
mfalme aitwe. Eliakimu mwana wa Hilkia
aliyekuwa msimamizi wa jumba la mfalme,
Shebna aliyekuwa katibu, na Yoa mwana
wa Asafu mwandishi wakawaendea.
19 [e]Yule jemadari wa jeshi akawaambia,
"Mwambieni Hezekia:

" 'Hili ndilo asemalo mfalme mkuu,
mfalme wa Ashuru: Ni wapi unapoweka
hili tumaini lako? 20 Unasema mnayo
mikakati na nguvu za kijeshi, lakini
unasema maneno matupu tu. Je, wewe
unamtegemea nani, hata ukaniasi
mimi? 21 [f]Tazama sasa, unaitegemea
Misri, fimbo ile ya mwanzi uliopasuka,
ambayo huuchoma na kuujeruhi
mkono wa mtu akiiegemea! Hivyo
ndivyo alivyo Farao mfalme wa Misri,
kwa wote wanaomtegemea. 22 Nawe
kama ukiniambia, "Tunamtumainia
BWANA Mungu wetu": je, siyo yeye
ambaye Hezekia aliondoa mahali
pake pa juu pa kuabudia miungu na
madhabahu zake, akiwaambia Yuda
na Yerusalemu, "Ni lazima mwabudu
mbele ya madhabahu haya katika
Yerusalemu"?
23 " 'Njooni sasa, fanyeni mapatano
na bwana wangu, mfalme wa Ashuru:
Nitakupa farasi elfu mbili, kama
unaweza kuwapandisha waendesha
farasi juu yao! 24 [g]Utawezaje kumzuia
hata afisa mmoja aliye mdogo kati
ya maafisa wa bwana wangu, ijapo
unategemea Misri kwa magari ya vita
na wapanda farasi? 25 [h]Zaidi ya hayo, je,
nimekuja kushambulia na kuangamiza
mahali hapa pasipo neno kutoka kwa
BWANA? BWANA mwenyewe ndiye
aliniambia niishambulie nchi hii na
kuiangamiza.' "

26 [i]Ndipo Eliakimu mwana wa Hilkia,
Shebna na Yoa wakamwambia yule
jemadari wa jeshi, "Tafadhali zungumza
na watumishi wako kwa lugha ya Kiaramu,
kwa kuwa tunaifahamu. Usiseme nasi
kwa Kiebrania watu walioko juu ya ukuta
wakiwa wanasikia."
27 Lakini yule jemadari wa jeshi akajibu,
"Je, bwana wangu amenituma kutoa
ujumbe huu kwa bwana wenu na kwenu
tu? Je, hakunituma pia kwa watu walioketi
ukutani, ambao, kama ninyi, itawabidi kula
mavi yao na kunywa mikojo yao wenyewe?"
28 Kisha yule jemadari wa jeshi akasimama
na kuita kwa lugha ya Kiebrania, akasema:
"Sikieni neno la mfalme mkuu, mfalme
wa Ashuru! 29 [j]Hili ndilo asemalo mfalme:
Msikubali Hezekia awadanganye. Hawezi
kuwaokoa mkononi mwangu. 30 Msikubali
Hezekia awashawishi kumtumaini
BWANA kwa kuwaambia, 'Hakika BWANA
atatuokoa. Mji huu hautaangukia mikononi
mwa mfalme wa Ashuru.'
31 [k]"Msimsikilize Hezekia. Hili ndilo
mfalme wa Ashuru asemalo: Fanyeni amani
nami na mje kwangu. Kisha kila mmoja
wenu atakula kutoka kwa mzabibu wake

[a]14 Talanta 30 za dhahabu ni sawa na tani moja.
[b]**18:15** 1Fal 15:18; Isa 39:2
[c]**18:17** 2Fal 20:20; Isa 20:1
[d]**18:18** 2Fal 19:2; Isa 22:20
[e]**18:19** Ay 4:6
[f]**18:21** Eze 29:6; Isa 30:5, 7
[g]**18:24** Isa 10:8
[h]**18:25** 2Fal 19:29
[i]**18:26** Ezr 4:7
[j]**18:29** 2Fal 19:10
[k]**18:31** Hes 13:23; Yer 14:3

na mtini wake mwenyewe, na kunywa maji
kutoka kisima chake mwenyewe, 32 [a]mpaka
nije nikawapeleke katika nchi iliyo kama
nchi yenu wenyewe, nchi ya nafaka na
divai mpya, nchi ya mkate na mashamba
ya mizabibu, nchi ya mizeituni na asali.
Chagueni uzima, sio mauti!

"Msimsikilize Hezekia, kwa kuwa
anawapotosha asemapo, 'BWANA
atatuokoa.' 33 [b]Je, yuko mungu wa taifa
lolote aliyewahi kuokoa nchi yake kutoka
mkononi mwa mfalme wa Ashuru? 34 [c]Iko
wapi miungu ya Hamathi na ya Arpadi?
Iko wapi miungu ya Sefarvaimu, Hena na
Iva? Je, imeokoa Samaria kutoka mkononi
mwangu? 35 [d]Ni yupi miongoni mwa miungu
yote ya nchi hizi ameweza kuokoa nchi
yake mkononi mwangu? Inawezekanaje
basi BWANA aiokoe Yerusalemu mkononi
mwangu?"

36 Lakini wale watu wakakaa kimya,
wala hawakujibu lolote, kwa kuwa mfalme
alikuwa amewaamuru, "Msimjibu lolote."

37 [e]Kisha Eliakimu mwana wa Hilkia
msimamizi wa jumba la kifalme, Shebna
katibu, na Yoa mwana wa Asafu, mwandishi
wakamwendea Hezekia, nguo zao zikiwa
zimeraruliwa, na kumwambia yale jemadari
wa jeshi aliyoyasema.

### *Hezekia Autafuta Msaada Wa BWANA*

**(Isaya 37:1-20)**

19 [f]Mfalme Hezekia aliposikia haya,
akararua nguo zake na kuvaa nguo
ya gunia, naye akaenda katika Hekalu
la BWANA. 2 [g]Akawatuma Eliakimu
msimamizi wa nyumba ya mfalme, Shebna
mwandishi, na viongozi wa makuhani,
wote wakiwa wamevaa nguo za magunia,
waende kwa nabii Isaya mwana wa Amozi.
3 [h]Wakamwambia, "Hili ndilo asemalo
Hezekia: Siku hii ni siku ya dhiki, ya
kukaripiwa na ya aibu, kama wakati watoto
wanapofikia karibu kuzaliwa na kumbe
hakuna nguvu ya kuwazaa. 4 [i]Yamkini
BWANA, Mungu wako atayasikia maneno
ya jemadari wa jeshi, ambaye bwana wake,
mfalme wa Ashuru, amemtuma kumdhihaki
Mungu aliye hai, tena kwamba atamkemea
kwa maneno ambayo BWANA, Mungu wako
ameyasikia. Kwa hiyo omba kwa ajili ya
mabaki ambao bado wako."

5 Maafisa wa Mfalme Hezekia walipofika
kwa Isaya, 6 [j]Isaya akawaambia,
"Mwambieni bwana wenu, 'Hili ndilo
asemalo BWANA: Usiogope kwa hayo
uliyoyasikia, yale maneno ambayo
watumishi wa mfalme wa Ashuru
wamenitukana nayo. 7 [k]Sikiliza! Nitatia
roho fulani ndani yake ili atakaposikia
taarifa fulani, atarudi nchi yake mwenyewe,
nami huko nitafanya auawe kwa upanga.' "

8 [l]Jemadari wa jeshi aliposikia kwamba
mfalme wa Ashuru ameondoka Lakishi,
alirudi, akamkuta mfalme akipigana na
Libna.

9 Basi Senakeribu akapata taarifa kwamba
Tirhaka, Mkushi mfalme wa Misri, alikuwa
anaenda kupigana naye. Basi akatuma
tena wajumbe kwa Hezekia na neno hili:
10 [m]"Mwambieni Hezekia mfalme wa Yuda:
Usikubali huyo Mungu unayemtumainia
akudanganye wakati anaposema,
'Yerusalemu haitatiwa mkononi mwa
mfalme wa Ashuru.' 11 Hakika umesikia yale
ambayo wafalme wa Ashuru wametenda
kwa nchi zote, wakiwaangamiza kabisa.
Je, wewe utaokolewa? 12 [n]Je, miungu ya
mataifa ambayo yaliangamizwa na baba
zangu iliweza kuwaokoa, hiyo miungu ya
Gozani, Harani, Resefu, na ya watu wa
Edeni waliokuwa Telasari? 13 [o]Yuko wapi
mfalme wa Hamathi, mfalme wa Arpadi,
mfalme wa mji wa Sefarvaimu, au wa Hena
au wa Iva?"

---

[a] **18:32** Kum 30:19
[b] **18:33** 2Fal 19:12
[c] **18:34** 2Fal 17:24; Isa 10:9
[d] **18:35** Za 2:1-2
[e] **18:37** Isa 33:7; 2Fal 6:30
[f] **19:1** Mwa 37:34; Hes 14:6
[g] **19:2** Yer 19:1; Mwa 37:34
[h] **19:3** Hos 13:13
[i] **19:4** 2Sam 16:12; Yer 37:3
[j] **19:6** Kum 3:2; Yos 1:9
[k] **19:7** Kut 14:24; 2Nya 32:21
[l] **19:8** 2Fal 18:14; Hes 33:20
[m] **19:10** 2Fal 18:5
[n] **19:12** 2Fal 18:33; Mwa 11:31
[o] **19:13** 2Fal 5:7

*Maombi Ya Hezekia*

14 [a]Hezekia akapokea barua kutoka kwa
wale wajumbe, naye akaisoma. Kisha
akapanda katika Hekalu la BWANA,
akaikunjua mbele za BWANA. 15 [b]Naye
Hezekia akamwomba BWANA akisema: "Ee
BWANA, Mungu wa Israeli, uketiye juu ya
kiti cha enzi kati ya makerubi, wewe peke
yako ndiwe Mungu juu ya falme zote za
dunia. Wewe umeumba mbingu na nchi.
16 [c]Tega sikio, Ee BWANA, usikie; fungua
macho yako, Ee BWANA, uone; sikiliza
maneno ambayo Senakeribu ametuma
kumtukana Mungu aliye hai.

17 "Ni kweli, Ee BWANA, kwamba
wafalme wa Ashuru wameyaangamiza
mataifa haya na nchi zao. 18 [d]Wameitupa
miungu yao kwenye moto na kuiangamiza,
kwa kuwa haikuwa miungu, bali miti na
mawe tu iliyotengenezwa kwa mikono ya
wanadamu. 19 [e]Sasa basi, Ee BWANA Mungu
wetu, tuokoe kutoka mkononi mwake, ili
falme zote duniani zipate kujua kwamba
wewe peke yako, Ee BWANA, ndiwe
Mungu."

*Isaya Anatoa Unabii Wa Kuanguka Kwa Senakeribu*

**(Isaya 37:21-38)**

20 [f]Kisha Isaya mwana wa Amozi
akapeleka ujumbe kwa Hezekia, akasema:
"Hili ndilo asemalo BWANA, Mungu wa
Israeli: Nimesikia maombi yako kuhusu
Senakeribu mfalme wa Ashuru. 21 [g]Hili ndilo
neno ambalo BWANA amelisema dhidi yake:

" 'Bikira Binti Sayuni anakudharau
na kukudhihaki.
Binti Yerusalemu anatikisa kichwa
chake unapokimbia.

22 [h]Ni nani uliyemtukana na
kumkufuru?
Ni nani uliyeinua sauti yako dhidi
yake,
na kumwinulia macho yako kwa
kiburi?
Ni dhidi ya yule Aliye Mtakatifu
wa Israeli!
23 [i]Kupitia kwa wajumbe wako
umelundika matukano juu ya
Bwana.
Nawe umesema,
"Kwa magari yangu mengi ya vita,
nimepanda juu ya vilele vya milima,
vilele vya juu sana katika
Lebanoni.
Nami nimeiangusha mierezi yake
mirefu,
misunobari yake iliyo bora sana.
Nimefikia sehemu zake zilizo mbali
sana,
misitu yake iliyo mizuri sana.
24 Nimechimba visima katika nchi za
kigeni
na kunywa maji yake.
Kwa nyayo za miguu yangu
nimekausha vijito vyote vya
Misri."

25 [j]" 'Je, hujasikia?
Zamani sana niliamuru hili.
Siku za kale nilipanga hili;
sasa nimelifanya litokee,
kwamba umegeuza miji yenye
ngome
kuwa malundo ya mawe.
26 [k]Watu wa miji hiyo wameishiwa
nguvu,
wanavunjika mioyo na
kuaibishwa.
Wao ni kama mimea katika shamba,
kama machipukizi mororo ya
kijani,
kama majani yachipuayo juu ya paa
la nyumba,
ambayo hukauka kabla ya kukua.

---

[a]**19:14** 2Fal 5:7
[b]**19:15** Mwa 3:24; Kut 25:22
[c]**19:16** Za 31:2; Kut 3:16
[d]**19:18** Yer 10:3-10; Mdo 17:29
[e]**19:19** 1Sam 12:10; Yos 4:24
[f]**19:20** 1Fal 9:3
[g]**19:21** Isa 47:1; Mao 2:13; Ay 16:4
[h]**19:22** Law 19:2; Hos 11:9
[i]**19:23** Za 20:7; Eze 31:3
[j]**19:25** Isa 22:11; Mik 1:6
[k]**19:26** Eze 7:17; Ay 8:12

27 [a]" 'Lakini ninajua mahali ukaapo,
kutoka kwako na kuingia kwako,
na jinsi unavyoghadhibika dhidi
yangu.
28 [b]Kwa sababu unaghadhibika dhidi
yangu,
na ufidhuli wako umefika
masikioni mwangu,
nitaweka ndoana yangu puani
mwako
na hatamu yangu kinywani
mwako,
nami nitakufanya urudi kwa njia
ile uliyoijia.'

29 [c]"Hii ndiyo itakuwa ishara kwako, ee
Hezekia:

"Mwaka huu utakula kile kiotacho
chenyewe,
na mwaka wa pili utakula kutoka
machipukizi yake.
Lakini katika mwaka wa tatu, panda
na uvune,
panda mashamba ya mizabibu na
ule matunda yake.
30 [d]Mara nyingine tena mabaki ya
nyumba ya Yuda
wataeneza mizizi chini na kuzaa
matunda juu.
31 [e]Kwa kuwa kutoka Yerusalemu
watakuja mabaki,
na kutoka Mlima Sayuni kundi la
walionusurika.

Wivu wa BWANA Mwenye Nguvu Zote ndio
utatimiza jambo hili.

32 "Kwa hiyo hili ndilo asemalo BWANA
kuhusu mfalme wa Ashuru:

"Hataingia katika mji huu
wala hatapiga mshale hapa.
Hatakuja mbele yake akiwa na ngao,
wala kupanga majeshi kuuzingira.
33 Kwa njia ile aliyoijia, ndiyo
atakayorudi;
hataingia katika mji huu,
asema BWANA.
34 [f]Nitaulinda mji huu na kuuokoa,
kwa ajili yangu mwenyewe,
na kwa ajili ya Daudi mtumishi
wangu."

35 [g]Usiku ule, malaika wa BWANA akaenda,
akawaua wanajeshi 185,000 katika kambi
ya Waashuru. Wenzao walipoamka asubuhi
yake, walikuta maiti kila mahali! 36 [h]Basi
Senakeribu mfalme wa Ashuru akavunja
kambi na kuondoka. Akarudi Ninawi na
kukaa huko.
37 [i]Siku moja, alipokuwa akiabudu katika
hekalu la mungu wake Nisroki, wanawe
Adrameleki na Shareza wakamuua kwa
upanga, nao wakakimbilia nchi ya Ararati.
Naye Esar-Hadoni mwanawe akawa mfalme
badala yake.

*Ugonjwa Wa Hezekia*

**(2 Nyakati 32:24-26; Isaya 38:1-8, 21-22)**

20 Katika siku hizo, Hezekia akaugua,
naye akawa karibu kufa. Nabii Isaya
mwana wa Amozi akaenda kwake na
kumwambia, "Hili ndilo asemalo BWANA:
Tengeneza mambo ya nyumba yako, kwa
sababu utakufa, hutapona."
2 Hezekia akaelekeza uso wake ukutani,
akamwomba BWANA: 3 [j]"Ee BWANA,
kumbuka jinsi nilivyoenenda mbele zako
kwa uaminifu na kujitoa kwa moyo wangu
wote, na kufanya yaliyo mema machoni
pako." Naye Hezekia akalia kwa uchungu.
4 Kabla Isaya hajaondoka katika ua wa
kati, neno la BWANA likamjia, akaambiwa:
5 [k]"Rudi ukamwambie Hezekia, kiongozi wa
watu wangu, 'Hili ndilo asemalo BWANA,
Mungu wa baba yako Daudi: Nimeyasikia
maombi yako na nimeona machozi yako;
nitakuponya. Siku ya tatu kuanzia sasa
utapanda kwenda Hekalu la BWANA.

[a]**19:27** Za 139:1-4
[b]**19:28** 2Nya 33:11; Eze 29:4
[c]**19:29** Lk 2:12; Za 107:37
[d]**19:30** Mwa 45:7; Amo 9:14
[e]**19:31** Mwa 45:7; Isa 9:7
[f]**19:34** 2Fal 20:6; 2Sam 7:15
[g]**19:35** Ay 24:24
[h]**19:36** Mwa 10:11
[i]**19:37** 2Fal 17:31; Mwa 8:4
[j]**20:3** Mwa 8:1; 2Nya 31:20
[k]**20:5** 1Fal 9:3; Za 39:12

6 [a]Nitakuongezea miaka kumi na mitano
katika maisha yako. Nami nitakuokoa wewe
pamoja na mji huu mkononi mwa mfalme
wa Ashuru. Nitaulinda mji huu kwa ajili
yangu, na kwa ajili ya mtumishi wangu
Daudi!' "
7 Kisha Isaya akasema, "Tengenezeni
dawa ya kubandika ya tini." Wakafanya
hivyo na kuiweka kwenye jipu, naye
akapona.
8 Hezekia alikuwa amemuuliza Isaya,
"Kutakuwa na ishara gani kwamba Bwana
ataniponya mimi, na kwamba nitapanda
kwenda Hekalu la Bwana siku ya tatu
tangu leo?"
9 [b]Isaya akajibu, "Hii ndiyo ishara ya
Bwana kwako kwamba Bwana atafanya
kile alichoahidi: Je, kivuli kiende hatua
kumi mbele, au kivuli kirudi nyuma hatua
kumi?"
10 [c]Hezekia akasema, "Ni jambo rahisi kwa
kivuli kutangulia mbele hatua kumi, kuliko
kukifanya kirudi nyuma hatua kumi."
11 [d]Ndipo nabii Isaya akamwita Bwana,
naye Bwana akakifanya kivuli kurudi
nyuma hatua kumi ambazo kilikuwa
kimeshuka kwenye ngazi ya Ahazi.

*Wajumbe Kutoka Babeli*

**(Isaya 39:1-8)**

12 Wakati huo Merodaki-Baladani, mwana
wa Baladani mfalme wa Babeli, akamtumia
Hezekia barua na zawadi, kwa sababu
alikuwa amesikia habari za kuugua kwa
Hezekia. 13 Hezekia akawapokea wale
wajumbe na kuwaonyesha vitu vyote
vile vilivyokuwa katika ghala zake: yaani
fedha, dhahabu, vikolezo na mafuta safi,
ghala la silaha na kila kitu kilichokuwa
katika hazina zake. Hapakuwa na kitu
chochote katika jumba lake la kifalme au
katika ufalme wake wote ambacho Hezekia
hakuwaonyesha.
14 Ndipo nabii Isaya akaenda kwa Mfalme
Hezekia na kumuuliza, "Watu hao walisema
nini, na wametoka wapi?"
Hezekia akamjibu, "Wametoka nchi ya
mbali. Walikuja kutoka Babeli."
15 Nabii akauliza, "Waliona nini katika
jumba lako la kifalme?"
Hezekia akajibu, "Waliona kila kitu
katika jumba langu la kifalme. Hakuna
kitu chochote katika hazina yangu ambacho
sikuwaonyesha."
16 Ndipo Isaya akamwambia Hezekia,
"Sikia neno la Bwana: 17 [e]Hakika wakati
unakuja ambapo vitu vyote katika jumba
lako la kifalme, na vyote ambavyo baba
zako waliweka akiba mpaka siku hii,
vitachukuliwa kwenda Babeli. Hakuna
chochote kitakachosalia, asema Bwana.
18 [f]Nao baadhi ya wazao wako, nyama yako
na damu yako mwenyewe watakaozaliwa
kwako, watachukuliwa mbali, nao
watakuwa matowashi katika jumba la
mfalme wa Babeli."
19 Hezekia akamjibu Isaya, "Neno la
Bwana ulilosema ni jema." Kwa kuwa
alifikiri, "Lakini si patakuwa na amani na
usalama wakati wa uhai wangu?"
20 Matukio mengine ya utawala wa
Hezekia, mafanikio yake yote, na jinsi
alivyotengeneza bwawa na mfereji ambao
ulileta maji katika mji, je, hayakuandikwa
katika kitabu cha kumbukumbu za wafalme
wa Yuda? 21 Hezekia akafa, akazikwa
pamoja na baba zake. Naye Manase
mwanawe akawa mfalme baada yake.

*Manase Mfalme Wa Yuda*

**(2 Nyakati 33:1-20)**

21 [g]Manase alikuwa na umri wa miaka
kumi na miwili alipoanza kutawala,
naye akatawala huko Yerusalemu miaka
hamsini na mitano. Mama yake aliitwa
Hefsiba. 2 [h]Akafanya maovu machoni pa
Bwana, akafuata desturi za machukizo
za mataifa ambayo Bwana aliyafukuza
mbele ya Waisraeli. 3 [i]Akajenga upya
mahali pa juu pa kuabudia miungu ambapo
Hezekia baba yake alikuwa amepabomoa.

[a]**20:6** 2Fal 19:34; 1Nya 17:19
[b]**20:9** Kum 13:2; Yer 44:29
[c]**20:10** 2Fal 3:18
[d]**20:11** Yos 10:13; 2Nya 32:31
[e]**20:17** 2Fal 24:13; Yer 52:17-23
[f]**20:18** 2Fal 24:15; Mik 4:10
[g]**21:1** 2Fal 21:16
[h]**21:2** Yer 15:4; 2Fal 16:3
[i]**21:3** Amu 6:28; Kum 17:3

Pia akasimamisha madhabahu za Baali
na kutengeneza nguzo ya Ashera, kama
Ahabu mfalme wa Israeli alivyofanya.
Akalisujudia jeshi lote la angani na
kuliabudu. 4 [a]Akajenga madhabahu katika
Hekalu la BWANA, ambamo BWANA alikuwa
amesema, “Katika Yerusalemu nitaliweka
Jina langu.” 5 [b]Katika nyua zote mbili za
Hekalu la BWANA, akajenga madhabahu
kwa ajili ya jeshi lote la angani. 6 [c]Akamtoa
kafara mwanawe mwenyewe katika moto,
akafanya uchawi na uaguzi, na akataka
shauri kwa wapiga ramli na kwa mizimu.
Akafanya maovu mengi sana machoni mwa
BWANA na kumghadhibisha.

7 [d]Akachukua nguzo ya Ashera
aliyoichonga na kuiweka katika Hekalu,
ambalo BWANA alikuwa amemwambia
Daudi na mwanawe Solomoni, “Katika
Hekalu hili na katika Yerusalemu
niliouchagua kutoka kabila zote za Israeli,
nitaliweka Jina langu milele. 8 [e]Sitaifanya
tena miguu ya Waisraeli itangetange
kutoka nchi niliyowapa baba zao, ikiwa
watakuwa waangalifu kufanya kila kitu
nilichowaamuru, na kuishika Sheria yote
ambayo walipewa na Mose mtumishi
wangu.” 9 [f]Lakini hawa watu hawakusikiliza.
Manase akawapotosha, hivyo kwamba
walifanya maovu mengi kuliko mataifa
ambayo BWANA aliyaangamiza mbele ya
Waisraeli.

10 BWANA akasema kupitia watumishi
wake manabii: 11 [g]“Manase mfalme wa
Yuda ametenda dhambi hizi za kuchukiza.
Amefanya maovu mengi kuliko Waamori
waliokuwepo kabla yake, na ameiongoza
Yuda katika dhambi kwa sanamu zake.
12 [h]Kwa hiyo hili ndilo asemalo BWANA,
Mungu wa Israeli: Nitaleta maafa makubwa
juu ya Yerusalemu na Yuda, kiasi kwamba
masikio ya kila mmoja atakayesikia habari
zake yatawasha. 13 [i]Nitanyoosha juu ya
Yerusalemu kamba ya kupimia iliyotumika
dhidi ya Samaria, na timazi iliyotumika
dhidi ya nyumba ya Ahabu. Nitaifutilia
mbali Yerusalemu kama mtu afutaye sahani,
nikiifuta na kuifunikiza. 14 [j]Nitawakataa
mabaki wa urithi wangu na kuwatia
mikononi mwa adui zao. Watapokonywa
mali zao na kutekwa nyara na adui zao
wote, 15 [k]kwa sababu wametenda uovu
machoni pangu na kunighadhibisha tangu
siku baba zao walipotoka Misri mpaka siku
ya leo.”

16 [l]Zaidi ya hayo, Manase pia alimwaga
damu nyingi isiyo na hatia, hivi kwamba
aliijaza Yerusalemu kutoka mwanzo hadi
mwisho, mbali na dhambi ambayo alikuwa
amesababisha Yuda kufanya, na hivyo
wakatenda maovu machoni pa BWANA.

17 Matukio mengine ya utawala wa
Manase, na yote aliyoyafanya, pamoja na
dhambi alizotenda, je, hayakuandikwa
katika kitabu cha kumbukumbu za wafalme
wa Yuda? 18 [m]Manase akalala pamoja na
baba zake na akazikwa katika bustani ya
jumba lake la kifalme, katika bustani ya
Uza. Naye Amoni mwanawe akawa mfalme
baada yake.

### *Amoni Mfalme Wa Yuda*

**(2 Nyakati 33:21-25)**

19 Amoni alikuwa na miaka ishirini
na miwili alipoanza kutawala, naye
akatawala huko Yerusalemu kwa miaka
miwili. Mamaye aliitwa Meshulemethi
binti Haruzi, kutoka Yotba. 20 [n]Akatenda
maovu machoni mwa BWANA, kama baba
yake Manase alivyofanya. 21 Akaenenda
katika njia zote za baba yake, akaabudu
sanamu ambazo baba yake aliziabudu
na kuzisujudia. 22 [o]Akamwacha BWANA,
Mungu wa baba zake, wala hakuenenda
katika njia za BWANA.

---

[a]**21:4** Isa 66:4; Kut 20:24
[b]**21:5** 1Fal 17:12
[c]**21:6** Law 18:21; Kum 18:14; 2Fal 23:26
[d]**21:7** Kum 16:21; Law 15:31; Kut 20:24
[e]**21:8** 2Sam 7:10
[f]**21:9** 1Fal 14:9; Eze 5:7
[g]**21:11** 1Fal 14:9; Mwa 15:6
[h]**21:12** Yer 15:4; 1Sam 3:11
[i]**21:13** Isa 34:11; Amo 7:7-9
[j]**21:14** 2Fal 19:4; Za 78:60
[k]**21:15** Yer 25:7
[l]**21:16** 2Fal 24:4; Mao 4:13; Sef 1:12
[m]**21:18** Es 1:5; 7:7
[n]**21:20** 1Fal 15:26
[o]**21:22** 1Fal 11:33; 1Sam 8:8

[23] Watumishi wa Amoni wakafanya fitina juu yake, nao wakamuulia kwake nyumbani. [24] Kisha watu wa nchi wakawaua wale wote waliokuwa wamefanya hila dhidi ya Mfalme Amoni. Wakamfanya Yosia mwanawe kuwa mfalme mahali pake.

[25] Matukio mengine ya utawala wa Amoni na yale aliyoyafanya, je, hayakuandikwa katika kitabu cha kumbukumbu za wafalme wa Yuda? [26] Akazikwa kwenye kaburi lake katika bustani ya Uza. Naye Yosia mwanawe akawa mfalme baada yake.

### *Yosia Mfalme Wa Yuda*

**(2 Nyakati 34; 35:20-27)**

22 [a]Yosia alikuwa na miaka minane alipoanza kutawala, naye akatawala huko Yerusalemu miaka thelathini na mmoja. Mama yake aliitwa Yedida binti Adaya, kutoka Boskathi. [2] [b]Akafanya yaliyo mema machoni pa BWANA na kuenenda katika njia zote za Daudi baba yake. Hakugeuka upande wa kuume wala wa kushoto.

[3] [c]Katika mwaka wa kumi na nane wa utawala wake, Mfalme Yosia akamtuma mwandishi Shafani mwana wa Azalia, mwana wa Meshulamu, kwenda katika Hekalu la BWANA. Akasema: [4] [d]"Panda uende kwa Hilkia, kuhani mkuu, umwambie ahesabu zile fedha ambazo zimeletwa katika Hekalu la BWANA, ambazo mabawabu wamekusanya kutoka kwa watu. [5] [e]Waambie waikabidhi kwa watu walioteuliwa kusimamia kazi ya Hekalu. Waamuru watu hawa wawalipe wafanyakazi ambao wanakarabati Hekalu la BWANA: [6] [f]wale maseremala, wajenzi na waashi. Waambie pia wanunue mbao na mawe yaliyochongwa ili kukarabati Hekalu. [7] [g]Lakini hawahitajiki kutoa hesabu ya fedha walizokabidhiwa, kwa sababu wanafanya kwa uaminifu."

[8] [h]Hilkia kuhani mkuu akamwambia Shafani mwandishi, "Nimekipata Kitabu cha Sheria ndani ya Hekalu la BWANA." Akampa Shafani, ambaye alikisoma. [9] Kisha Shafani mwandishi akamwendea mfalme na kumpa taarifa akisema: "Maafisa wako wametoa ile fedha ambayo ilikuwa ndani ya Hekalu la BWANA na imekabidhiwa mikononi mwa wasimamizi wa marekebisho ya Hekalu." [10] [i]Ndipo Shafani mwandishi akampasha mfalme habari kwamba: "Hilkia kuhani amenipa kitabu hiki." Naye Shafani akakisoma kile kitabu mbele ya mfalme.

[11] Mfalme aliposikia maneno ya kile Kitabu cha Sheria, akararua mavazi yake. [12] [j]Akatoa maagizo haya kwa Hilkia kuhani, Ahikamu mwana wa Shafani, Akbori mwana wa Mikaya, Shafani mwandishi, na Asaya mtumishi wa mfalme: [13] [k]"Nendeni mkamuulize BWANA kwa ajili yangu, na kwa ajili ya watu na Yuda wote kuhusu yale yaliyoandikwa ndani ya kitabu hiki ambacho kimepatikana. Hasira ya BWANA ni kubwa inayowaka dhidi yetu kwa sababu baba zetu hawakuyatii maneno ya kitabu hiki. Hawajatenda kulingana na yale yote yaliyoandikwa humo kutuhusu sisi."

[14] [l]Hilkia kuhani, Ahikamu, Akbori, Shafani na Asaya wakaenda kuongea na nabii mke Hulda, ambaye alikuwa mke wa Shalumu mwana wa Tikwa, mwana wa Harhasi mtunzaji wa chumba cha mavazi. Hulda aliishi Yerusalemu katika Mtaa wa Pili.

[15] Akawaambia, "Hivi ndivyo asemavyo BWANA, Mungu wa Israeli: Mwambieni yule mtu aliyewatuma ninyi kwangu, [16] [m]'Hivi ndivyo asemavyo BWANA: Nitaleta maafa juu ya mahali hapa na watu wake, kulingana na kila kitu kilichoandikwa katika kitabu hicho mfalme wa Yuda alichosoma. [17] [n]Kwa sababu wameniacha mimi na kufukiza uvumba kwa miungu

---

[a]**22:1** Yer 1:2; Yos 15:39
[b]**22:2** Kum 5:32
[c]**22:3** 2Nya 34:20; Yer 39:14
[d]**22:4** Ezr 7:1; 2Fal 12:4-5
[e]**22:5** 2Fal 12:5
[f]**22:6** 2Fal 12:11-12
[g]**22:7** 2Fal 12:15
[h]**22:8** Kum 31:24; Gal 3:10
[i]**22:10** Yer 36:21
[j]**22:12** 2Fal 25:22; Isa 8:14
[k]**22:13** Kum 29:24-28; Amo 2:4
[l]**22:14** Kut 15:20
[m]**22:16** Yos 23:15; Dan 9:11
[n]**22:17** 1Fal 9:9

mingine, na kunighadhibisha kwa sanamu
zote zilizotengenezwa kwa mikono yao,
hasira yangu itawaka dhidi ya mahali
hapa, wala haitatulizwa.’ 18 [a]Mwambieni
mfalme wa Yuda, ambaye amewatuma
kumuuliza BWANA, ‘Hivi ndivyo asemavyo
BWANA, Mungu wa Israeli, kuhusu maneno
uliyoyasikia: 19 [b]Kwa kuwa moyo wako
ulikuwa msikivu na ulijinyenyekeza mbele
za BWANA uliposikia kile nilichosema dhidi
ya mahali hapa na watu wake, kwamba
wangelaaniwa na kuachwa ukiwa, basi kwa
sababu uliyararua mavazi yako na kulia
mbele zangu, nimekusikia, asema BWANA.
20 [c]Kwa hiyo nitakukusanya kwa baba zako,
nawe utazikwa kwa amani. Macho yako
hayataona maafa yote nitakayoleta juu ya
mahali hapa.’ ”

Basi wakapeleka jibu lake kwa mfalme.

*Yosia Analifanya Upya Agano*

**(2 Nyakati 34:3-7, 29-33)**

23 Kisha mfalme akawaita pamoja
wazee wote wa Yuda na Yerusalemu.
2 [d]Akapanda kwenda hekaluni mwa
BWANA pamoja na watu wa Yuda, watu
wa Yerusalemu, makuhani na manabii,
watu wote wakubwa kwa wadogo.
Akasoma wakiwa wanasikia maneno yote
ya Kitabu cha Agano, ambacho kilikuwa
kimepatikana katika Hekalu la BWANA.
3 [e]Mfalme akasimama karibu na nguzo, na
kufanya upya agano mbele za BWANA: yaani
kumfuata BWANA na kuzishika amri zake,
maagizo na sheria kwa moyo wake wote na
kwa roho yake yote, hivyo kuyathibitisha
maneno ya agano yaliyoandikwa katika
kitabu hiki. Kisha watu wote wakajifunga
wenyewe kwa kiapo katika agano.

4 [f]Mfalme akamwamuru Hilkia kuhani
mkuu, makuhani waliomfuata kwa cheo, na
mabawabu kuondoa kutoka kwenye Hekalu
la BWANA vyombo vyote vilivyofanywa kwa
ajili ya Baali na Ashera na jeshi lote la mianga
ya angani! Akavichoma nje ya Yerusalemu
katika mashamba ya Bonde la Kidroni, na
kuyachukua hayo majivu mpaka Betheli.
5 [g]Akawafukuza makuhani wa kipagani
waliokuwa wameteuliwa na wafalme wa
Yuda kufukiza uvumba katika mahali pa
juu pa kuabudia miungu katika miji ya
Yuda na ile iliyozunguka Yerusalemu, yaani
wale waliofukiza uvumba kwa Baali, kwa
jua na mwezi, kwa makundi ya nyota, na
jeshi lote la angani. 6 [h]Akaiondoa nguzo ya
Ashera kutoka kwenye Hekalu la BWANA,
na kuipeleka kwenye Bonde la Kidroni
nje ya Yerusalemu, akaiteketeza huko.
Akaisaga hadi ikawa unga na kusambaza
hilo vumbi juu ya makaburi ya watu wa
kawaida. 7 [i]Akabomoa pia nyumba za
mahanithi wa mahali pa ibada za miungu,
zilizokuwa ndani ya Hekalu la BWANA na
mahali wanawake walipofuma kwa ajili ya
Ashera.

8 [j]Yosia akawaleta makuhani wote wa
BWANA kutoka miji yote ya Yuda, na
kunajisi mahali pa juu pa kuabudia miungu,
kuanzia Geba hadi Beer-Sheba, mahali
pote ambapo hao makuhani wa miungu
walifukiza uvumba. Akabomoa mahali
pa kuwekea vitu vya ibada za miungu
palipokuwa katika malango, kwenye
ingilio la Lango la Yoshua, mtawala wa mji,
lililoko upande wa kushoto wa lango la mji.
9 [k]Ingawa makuhani wa mahali pa juu pa
kuabudia miungu hawakuhudumu katika
madhabahu ya BWANA katika Yerusalemu,
walikula mikate isiyotiwa chachu miongoni
mwa ndugu zao.

10 [l]Kisha mfalme akanajisi Tofethi,
palipokuwa katika Bonde la Ben-Hinomu,
ili mtu yeyote asiweze kupatumia kumtoa
kafara mwanawe au binti yake katika moto
kwa mungu Moleki. 11 [m]Akaondoa kutoka
kwenye ingilio la Hekalu la BWANA wale
farasi ambao wafalme wa Yuda walikuwa

[a]**22:18** Yer 21:2
[b]**22:19** Isa 37:15; Yer 26:6; Law 26:31
[c]**22:20** Isa 47:11; 1Fal 21:29
[d]**23:2** Kum 31:11; Kut 24:7
[e]**23:3** 1Fal 7:15; Kum 13:4
[f]**23:4** 2Fal 25:18; Yer 35:4
[g]**23:5** 2Fal 16:4; Yer 8:2
[h]**23:6** Kut 32:20; Yer 26:23
[i]**23:7** 1Fal 14:24; Eze 16:16
[j]**23:8** 1Fal 15:22
[k]**23:9** Eze 44:10-14
[l]**23:10** Law 18:21; Isa 30:33
[m]**23:11** Neh 9:34; Kum 4:19

wamewaweka wakfu kwa ajili ya jua.
Walikuwa kwenye ua karibu na chumba cha
afisa aliyeitwa Nathan-Meleki. Basi Yosia
akayachoma moto yale magari yaliyokuwa
yamewekwa wakfu kwa jua.
12 [a]Alizivunja madhabahu ambazo
wafalme wa Yuda walikuwa wamezijenga
kwenye paa la ghorofa ya Ahazi, pia
madhabahu alizokuwa amezijenga Manase
katika nyua mbili za Hekalu la Bwana.
Akaziondoa huko, akazivunja vipande
vipande, na kutupa hicho kifusi katika
Bonde la Kidroni. 13 [b]Mfalme pia akanajisi
mahali pa juu pa kuabudia miungu,
palipokuwa mashariki ya Yerusalemu
upande wa kusini wa Kilima cha Uharibifu,
pale ambapo Solomoni mfalme wa Israeli
alikuwa amejenga kwa ajili ya Ashtorethi
mungu mke chukizo la Wasidoni, kwa ajili
ya Kemoshi mungu chukizo la Wamoabu,
na kwa ajili ya Moleki mungu chukizo la
watu wa Amoni. 14 [c]Yosia akapasua yale
mawe ya kuabudiwa na kuzikatakata nguzo
za Ashera. Kisha akafunika hayo maeneo
kwa mifupa ya wanadamu.
15 [d]Hata madhabahu yaliyokuwa huko
Betheli, mahali pa juu pa kuabudia miungu
palipokuwa pamejengwa na Yeroboamu
mwana wa Nebati, ambaye aliwafanya
Israeli watende dhambi, alibomoa hata
hayo madhabahu na mahali pa juu pa
kuabudia miungu. Alipateketeza kwa moto
hapo mahali pa juu pa kuabudia miungu na
kupasaga hadi pakawa vumbi, na kuichoma
hiyo nguzo ya Ashera pia. 16 [e]Kisha Yosia
akatazama huku na huko, naye alipoona
makaburi yaliyokuwa huko kwenye
kilima, akaamuru mifupa itolewe humo na
akaichoma juu ya madhabahu ya Betheli ili
kupanajisi. Hili lilitokea kulingana na neno
la Bwana lililosemwa na mtu wa Mungu
ambaye alitangulia kusema mambo haya.
17 Mfalme akauliza, "Lile kaburi lenye
mnara wa ukumbusho ninaloliona ni kwa
ajili gani?"
Watu wa mji wakasema, "Hii ni alama
ya kaburi la mtu wa Mungu aliyekuja
kutoka Yuda, naye akanena dhidi ya hii
madhabahu ya Betheli mambo yale yale
uliyoifanyia leo."
18 [f]Akasema, "Liacheni, msiliguse.
Msimruhusu mtu yeyote kuiondoa mifupa
yake." Basi wakaiacha mifupa yake pamoja
na ile ya yule nabii ambaye alikuwa
amekuja kutoka Samaria.
19 Kama alivyokuwa amefanya huko
Betheli, Yosia akabomoa na kunajisi mahali
pa kuabudia miungu kwenye mahali pa
juu ambapo wafalme wa Israeli walikuwa
wamejenga ndani ya miji ya Samaria,
ambayo ilikuwa imemghadhibisha Bwana.
20 [g]Yosia akawachinja makuhani wote wa
mahali pa juu pa kuabudia miungu katika
madhabahu zao wenyewe, na kuchoma
mifupa ya wanadamu juu yake. Kisha
akarudi Yerusalemu.

*Yosia Aadhimisha Pasaka*

21 [h]Mfalme akatoa agizo hili kwa watu
wote: "Adhimisheni Pasaka kwa Bwana
Mungu wenu, kama ilivyoandikwa katika
Kitabu hiki cha Agano." 22 Hapakuwahi
kuwepo na adhimisho lingine la Pasaka
kama hilo tangu nyakati za Waamuzi
walioongoza Israeli, wala katika nyakati
zote za wafalme wa Israeli na wafalme wa
Yuda. 23 [i]Lakini katika mwaka wa kumi
na nane wa utawala wa Mfalme Yosia,
Pasaka hii iliadhimishwa kwa Bwana huko
Yerusalemu.
24 [j]Zaidi ya hayo, Yosia akawaondoa
waaguzi, wanaoabudu mizimu, sanamu
za kuagulia, sanamu za kuabudiwa,
na vitu vingine vyote vya machukizo
vilivyoonekana huko Yuda na Yerusalemu.
Aliyafanya haya ili kutimiza matakwa ya
sheria iliyoandikwa ndani ya kile kitabu
ambacho Hilkia kuhani alikipata ndani ya
Hekalu la Bwana. 25 [k]Kabla wala baada

[a]**23:12** 2Nya 33:15; Yer 19:13
[b]**23:13** 1Fal 11:7; Kum 27:15
[c]**23:14** Kut 23:24; Za 53:5
[d]**23:15** 1Fal 12:33; Yos 7:2
[e]**23:16** 1Fal 13:2
[f]**23:18** 1Fal 13:31
[g]**23:20** 2Fal 11:18; Kut 22:20
[h]**23:21** Kut 12:11
[i]**23:23** Hes 28:16
[j]**23:24** Kum 18:11; Mwa 31:19
[k]**23:25** 1Sam 7:3

ya Mfalme Yosia hapakuwepo na mfalme mwingine yeyote ambaye alimpenda BWANA kwa moyo wake wote, kwa roho yake yote, na kwa nguvu zake zote, sawasawa na Sheria yote ya Mose.
26 [a]Hata hivyo, BWANA hakuacha ghadhabu yake iliyowaka dhidi ya Yuda kwa sababu ya yale yote ambayo Manase alikuwa amefanya kumghadhibisha.
27 [b]Hivyo BWANA akasema, "Nitamwondoa Yuda mbele zangu kama nilivyomwondoa Israeli, nami nitaukataa Yerusalemu, mji niliouchagua, na Hekalu hili, ambalo nilisema, 'Jina langu litakaa humo.' "
28 Matukio mengine ya utawala wa Yosia na yote aliyoyafanya, je, hayakuandikwa katika kitabu cha kumbukumbu za wafalme wa Yuda?
29 [c]Yosia alipokuwa mfalme, Farao Neko mfalme wa Misri akapanda mpaka Mto Frati kumsaidia mfalme wa Ashuru. Mfalme Yosia akatoka kwenda kupigana naye, lakini Neko akamkabili na kumuua huko
Megido. 30 [d]Watumishi wa Yosia wakauleta mwili wake katika gari la vita kutoka Megido hadi Yerusalemu, wakamzika kwenye kaburi lake mwenyewe. Nao watu wa nchi wakamchukua Yehoahazi mwana wa Yosia, wakamtia mafuta na kumfanya mfalme mahali pa baba yake.

*Yehoahazi Mfalme Wa Yuda*

**(2 Nyakati 36:2-4)**

31 [e]Yehoahazi alikuwa na umri wa miaka ishirini na mitatu alipoanza kutawala, naye akatawala huko Yerusalemu kwa miezi mitatu. Jina la mama yake aliitwa Hamutali binti Yeremia kutoka Libna.
32 [f]Akafanya maovu machoni mwa BWANA,
kama baba zake walivyofanya. 33 [g]Farao
Neko akamfunga kwa minyororo huko Ribla katika nchi ya Hamathi ili asiweze kutawala huko Yerusalemu, naye akatoza kodi ya talanta mia moja[h] za fedha, na talanta
moja ya dhahabu[i] katika Yuda. 34 [j]Farao
Neko akamfanya Eliakimu mwana wa Yosia kuwa mfalme mahali pa baba yake Yosia, na kulibadilisha jina la Eliakimu kuwa Yehoyakimu. Lakini akamchukua Yehoahazi na kumpeleka Misri, naye akafia huko.

*Yehoyakimu Mfalme Wa Yuda*

**(2 Nyakati 36:5-8)**

35 Yehoyakimu akamlipa Farao Neko ile fedha na dhahabu aliyodai. Ili kuweza kufanya hivyo, Yehoyakimu akatoza nchi kodi na kulipiza fedha na dhahabu kutoka kwa watu wa nchi kulingana na makadrio ya mapato yao.
36 Yehoyakimu alikuwa na umri wa miaka ishirini na mitano alipoanza kutawala, naye akatawala huko Yerusalemu miaka kumi na mmoja. Jina la mama yake aliitwa
Zebida binti Pedaya kutoka Ruma. 37 Naye
akafanya maovu machoni mwa BWANA, kama baba zake walivyokuwa wamefanya.
24 [k]Wakati wa utawala wa Yehoyakimu, Nebukadneza mfalme wa Babeli aliishambulia nchi, naye Yehoyakimu akawa mtumwa wake kwa miaka mitatu. Lakini hatimaye akabadili mawazo yake na kuasi
dhidi ya Nebukadneza. 2 [l]BWANA akatuma
wavamiaji wa Wakaldayo, Waaramu, Wamoabu na Waamoni ili kumshambulia. Aliwatuma kuiangamiza Yuda sawasawa na neno la BWANA lililosemwa na watumishi
wake manabii. 3 [m]Hakika mambo haya
yalitokea Yuda kulingana na agizo la BWANA, ili kuwaondoa kutoka machoni pake kwa sababu ya dhambi za Manase
na yote aliyoyafanya, 4 [n]ikiwa ni pamoja
na kumwaga damu isiyo na hatia. Kwa kuwa aliijaza Yerusalemu kwa damu isiyo

[a]**23:26** 2Fal 21:12
[b]**23:27** Kut 33:15; Yer 27:10
[c]**23:29** Yer 46:2; 2Fal 9:27
[d]**23:30** 2Fal 9:28
[e]**23:31** 1Nya 3:15; Yer 22:11
[f]**23:32** 1Fal 15:26
[g]**23:33** Hes 34:11; 1Fal 8:65

[h]33 Talanta 100 za fedha ni sawa na tani 3.4.
[i]33 Talanta moja ya dhahabu ni sawa na kilo 34.
[j]**23:34** 2Nya 36:5-8; Yer 22:12
[k]**24:1** Yer 25:1, 9; 2Fal 18:7
[l]**24:2** Yer 5:15; Isa 28:18-19; Eze 23:23
[m]**24:3** 2Fal 21:12
[n]**24:4** 2Fal 21:16; Kut 23:21

na hatia, naye BWANA hakuwa radhi
kusamehe.
5 [a]Matukio mengine ya utawala wa
Yehoyakimu na yote aliyoyafanya,
je, hayakuandikwa katika kitabu cha
kumbukumbu za wafalme wa Yuda?
6 [b]Yehoyakimu akalala pamoja na baba
zake. Naye Yehoyakini mwanawe akawa
mfalme baada yake.
7 [c]Mfalme wa Misri hakutoka tena katika
nchi yake, kwa sababu mfalme wa Babeli
alikuwa ameitwaa himaya yake yote,
kuanzia Kijito cha Misri hadi Mto Frati.

*Yehoyakini Mfalme Wa Yuda*

**(2 Nyakati 36:9-10)**

8 [d]Yehoyakini alikuwa na miaka kumi
na minane alipoanza kutawala, naye
akatawala huko Yerusalemu miezi mitatu.
Jina la mama yake aliitwa Nehushta binti
Elnathani kutoka Yerusalemu. 9 [e]Akafanya
maovu machoni pa BWANA, kama vile baba
yake alivyokuwa amefanya.
10 [f]Wakati huo, maafisa wa Nebukadneza
mfalme wa Babeli walikuja ili kuishambulia
Yerusalemu, nao wakaizunguka kwa jeshi.
11 Nebukadneza mwenyewe akaupandia
mji wakati maafisa wake walipokuwa
wameuzunguka kwa jeshi. 12 [g]Yehoyakini
mfalme wa Yuda, mama yake, wahudumu
wake, wakuu na maafisa wake wote
wakajisalimisha kwa Nebukadneza.
Katika mwaka wa nane wa utawala wa
mfalme wa Babeli, akamchukua Yehoyakini
kuwa mfungwa. 13 [h]Kama vile BWANA
alivyokuwa amesema, Nebukadneza
akaondoa hazina yote kutoka Hekalu
la BWANA na kutoka jumba la mfalme,
akavichukua vyombo vyote vya dhahabu
ambavyo Solomoni mfalme wa Israeli
alikuwa amevitengeneza kwa ajili ya
Hekalu la BWANA. 14 [i]Akawachukua watu
wa Yerusalemu wote kwenda uhamishoni:
yaani maafisa wote na mashujaa, watu
wenye ustadi na ufundi, jumla yao watu
elfu kumi. Watu maskini sana ndio tu
waliobaki katika nchi.
15 [j]Nebukadneza akamchukua mateka
Yehoyakini hadi Babeli. Pia akawachukua
utumwani kutoka Yerusalemu hadi
Babeli mama yake mfalme, wake zake,
maafisa wake, na viongozi wote wa nchi.
16 [k]Mfalme wa Babeli pia akawahamishia
Babeli mashujaa elfu saba, wenye nguvu
na wanaofaa kupigana vita, na watu wenye
ustadi na mafundi elfu moja. 17 [l]Akamfanya
Matania, ndugu wa baba yake Yehoyakini,
kuwa mfalme mahali pake, na akalibadilisha
jina lake kuwa Sedekia.

*Sedekia Mfalme Wa Yuda*

**(2 Nyakati 36:11-12; Yeremia 52:1-3)**

18 [m]Sedekia alikuwa na umri wa miaka
ishirini na mmoja alipoanza kutawala,
naye akatawala huko Yerusalemu miaka
kumi na mmoja. Jina la mama yake aliitwa
Hamutali binti Yeremia, kutoka Libna.
19 Alifanya maovu machoni pa BWANA,
kama alivyofanya Yehoyakimu. 20 Ilikuwa
ni kwa sababu ya hasira ya BWANA haya
yote yalitokea Yerusalemu na Yuda, naye
mwishoni akawaondoa mbele zake.
Basi, Sedekia akaasi dhidi ya mfalme wa
Babeli.

*Kuanguka Kwa Yerusalemu*

**(2 Nyakati 36:13-21; Yeremia 52:3-30)**

25 [n]Hivyo katika mwaka wa tisa wa
utawala wa Sedekia, katika siku ya
kumi ya mwezi wa kumi, Nebukadneza
mfalme wa Babeli, akiwa na jeshi lake
lote, alifanya vita dhidi ya Yerusalemu.
Akapiga kambi nje ya mji na kuuzunguka

---

[a]**24:5** Yer 22:18-19
[b]**24:6** Yer 22:19; Eze 19:1
[c]**24:7** Mwa 15:18; Yer 46:25
[d]**24:8** 1Nya 3:16; Yer 13:18
[e]**24:9** 1Fal 15:26
[f]**24:10** 2Fal 24:1
[g]**24:12** Yer 24:1
[h]**24:13** 2Fal 20:17; Isa 39:6
[i]**24:14** Kum 28:36; Ay 5:16
[j]**24:15** 2Fal 20:18; Mao 2:9
[k]**24:16** Ezr 2:1
[l]**24:17** 2Nya 36:11; Yer 37:1
[m]**24:18** Yer 39:1; 2Fal 23:31
[n]**25:1** Yer 21:2; Eze 21:22

mji pande zote. 2 Mji ulizungukwa na jeshi
mpaka mwaka wa kumi na moja wa utawala
wa Mfalme Sedekia. 3 [a]Ilipowadia siku ya
tisa ya mwezi wa nne, njaa ikazidi kuwa
kali sana ndani ya mji, hadi hapakuwa na
chakula kwa ajili ya watu. 4 [b]Kisha ukuta
wa mji ukavunjwa, na jeshi lote likakimbia.
Wakaondoka mjini usiku kupitia lango
lililokuwa kati ya kuta mbili karibu na
bustani ya mfalme, ingawa Wakaldayo
walikuwa wameuzunguka mji. Wakakimbia
kuelekea Araba. 5 [c]Lakini jeshi la Wakaldayo
likamfuatia mfalme na kumpata katika
sehemu tambarare za Yeriko. Askari wake
wote wakatengwa naye na kutawanyika,
6 [d]naye akakamatwa. Akapelekwa kwa
mfalme wa Babeli huko Ribla, mahali
ambapo hukumu yake ilitangazwa.
7 [e]Wakawaua wana wa Sedekia mbele ya
macho yake. Kisha wakayang'oa macho
yake, wakamfunga kwa pingu za shaba na
kumpeleka Babeli.

8 Mnamo siku ya saba ya mwezi wa tano,
katika mwaka wa kumi na tisa wa utawala
wa Nebukadneza mfalme wa Babeli,
Nebuzaradani jemadari wa askari walinzi
wa mfalme, afisa wa mfalme wa Babeli,
alikuja Yerusalemu. 9 [f]Alichoma moto
Hekalu la Bwana, jumba la kifalme, na
nyumba zote za Yerusalemu. Aliteketeza kila
jengo muhimu. 10 [g]Jeshi lote la Wakaldayo,
chini ya jemadari wa askari walinzi wa
mfalme, walivunja kuta zilizoizunguka
Yerusalemu. 11 [h]Nebuzaradani jemadari
wa askari walinzi akawapeleka uhamishoni
watu waliokuwa wamebaki katika mji,
pamoja na mabaki ya watu wa kawaida,
na wale waliojisalimisha kwa mfalme wa
Babeli. 12 [i]Lakini yule jemadari wa askari
walinzi akawaacha baadhi ya wale watu
maskini kabisa ili watunze mashamba ya
mizabibu na mashamba mengine.

13 Wakaldayo walivunja vipande zile
nguzo za shaba, vile vishikilio vya shaba
vilivyohamishika, na ile Bahari ya shaba,
ambavyo vyote vilikuwa katika Hekalu la
Bwana. Hivyo wakaichukua hiyo shaba
na kuipeleka Babeli. 14 [j]Wakachukua pia
vyungu, masepetu, mikasi ya kusawazishia
tambi, sahani na vyombo vyote vya shaba
vilivyotumika katika huduma ya Hekalu.
15 [k]Jemadari wa askari walinzi wa mfalme
akachukua vile vyetezo na yale mabakuli
ya kunyunyizia, vitu vyote vile vilivyokuwa
vimetengenezwa kwa dhahabu safi au
fedha.

16 Shaba iliyotokana na zile nguzo mbili,
ile Bahari na vile vishikilio vilivyohamishika,
ambavyo Solomoni alikuwa ametengeneza
kwa ajili ya Hekalu la Bwana, ilikuwa na
uzito usioweza kupimika. 17 [l]Kila nguzo
ilikuwa na urefu wa dhiraa kumi na nane.[m]
Sehemu ya shaba juu ya nguzo moja
ilikuwa na urefu wa dhiraa tatu[n] na ilikuwa
imepambwa kwa wavu na makomamanga
ya shaba kuizunguka kote. Ile nguzo
nyingine pamoja na wavu wake ilifanana
na hiyo ya kwanza.

18 [o]Yule jemadari wa askari walinzi
akawachukua kama wafungwa Seraya
kuhani mkuu, kuhani Sefania aliyefuata kwa
cheo, na mabawabu watatu. 19 Miongoni
mwa wale watu waliokuwa wamesalia
katika mji, alimchukua afisa kiongozi
wa wapiganaji, na washauri watano wa
mfalme. Akamchukua pia mwandishi
aliyesimamia uandikishaji wa watu wa nchi,
pamoja na watu wake sitini waliopatikana
ndani ya mji. 20 Nebuzaradani jemadari
akawachukua hao wote na kuwapeleka
kwa mfalme wa Babeli huko Ribla. 21 [p]Huko
Ribla, katika nchi ya Hamathi, mfalme wa
Babeli akaamuru wanyongwe.

---

[a]**25:3** Law 26:26; Mao 2:20
[b]**25:4** Ay 30:14; Eze 33:21
[c]**25:5** Law 26:36; Eze 12:14
[d]**25:6** Isa 22:3; Hes 34:11
[e]**25:7** Kum 28:36; Eze 40:1
[f]**25:9** Za 74:3-8; Amo 2:5
[g]**25:10** Yer 50:15
[h]**25:11** Law 26:44; 2Fal 24:14
[i]**25:12** 2Fal 24:14
[j]**25:14** Hes 7:14; Ezr 1:7
[k]**25:15** 2Fal 24:13; Yer 15:13
[l]**25:17** 1Fal 7:15-22
[m]17 Dhiraa 18 ni sawa na mita 8.2.
[n]17 Dhiraa 3 ni sawa na mita 1.35.
[o]**25:18** 1Nya 6:14; Yer 21:1
[p]**25:21** Hes 34:11

Hivyo Yuda wakaenda utumwani, mbali na nchi yao.
22 [a]Nebukadneza mfalme wa Babeli akamteua Gedalia mwana wa Ahikamu, mwana wa Shafani, awe msimamizi wa
watu aliowaacha Yuda. 23 Maafisa wote
wa jeshi na watu wao waliposikia kwamba mfalme wa Babeli amemteua Gedalia kuwa mtawala, wakamjia Gedalia huko Mispa. Hawa walikuwa Ishmaeli mwana wa Nethania, Yohanani mwana wa Karea, Seraya mwana wa Tanhumethi Mnetofathi, na Yezania mwana wa Mmaaka, pamoja na
watu wao. 24 Gedalia akaapa ili kuwatia
moyo wao na watu wao. Akasema, "Msiwaogope maafisa wa Kikaldayo. Kaeni katika nchi na kumtumikia mfalme wa Babeli, na itakuwa vyema kwenu."
25 [b]Hata hivyo, katika mwezi wa saba Ishmaeli mwana wa Nethania mwana wa Elishama, aliyekuwa wa uzao wa mfalme, akaja pamoja na watu kumi, nao wakamuua Gedalia, na pia watu wa Yuda, pamoja na Wakaldayo waliokuwa naye huko Mispa.
26 [c]Baada ya haya, watu wote kuanzia aliye mdogo sana hadi aliye mkubwa kabisa, pamoja na maafisa wa jeshi, wakakimbilia Misri kwa kuwaogopa Wakaldayo.

*Yehoyakini Anaachiwa*

**(Yeremia 52:31-34)**

27 [d]Katika mwaka wa thelathini na saba tangu Yehoyakini mfalme wa Yuda apelekwe uhamishoni, katika mwaka ule ambao Evil-Merodaki[e] alifanyika mfalme wa Babeli, alimwacha huru Yehoyakini kutoka gerezani siku ya ishirini na saba ya mwezi
wa kumi na mbili. 28 [f]Alizungumza naye
kwa upole na kumpa kiti cha heshima zaidi kuliko wale wafalme wengine aliokuwa nao
huko Babeli. 29 [g]Hivyo Yehoyakini akayavua
mavazi yake ya mfungwa, na siku zote za maisha yake zilizobaki alikula mezani mwa
mfalme. 30 [h]Siku kwa siku mfalme alimpa
Yehoyakini posho siku zote za maisha yake.

[a]**25:22** Yer 40:5, 7; 2Fal 22:12
[b]**25:25** 2Fal 12:20; Zek 7:5
[c]**25:26** Isa 30:2; Yer 43:7
[d]**25:27** 2Fal 24:12
[e]27 Pia aliitwa Ameli-Mariduki.
[f]**25:28** Ezr 5:5; Dan 2:48
[g]**25:29** 2Sam 9:7
[h]**25:30** Mwa 43:34; Es 9:22

# 1 MAMBO YA NYAKATI

*Kumbukumbu Za Historia Kuanzia Adamu Hadi Abrahamu*

**(Mwanzo 5:1-32; 10:1-32; 11:10-26)**

*Adamu Hadi Wana Wa Noa*

1 [a]Adamu, Sethi, Enoshi, 2 [b]Kenani,
Mahalaleli, Yaredi, 3 [c]Enoki, Methusela,
Lameki, Noa.

4 [d]Wana wa Noa walikuwa:
Shemu, Hamu na Yafethi.

*Wana Wa Yafethi*

5 Wana wa Yafethi walikuwa:
Gomeri, Magogu, Madai, Yavani, Tubali, Mesheki na Tirasi.
6 Wana wa Gomeri walikuwa:
Ashkenazi, Rifathi na Togarma.
7 Wana wa Yavani walikuwa:
Elisha, Tarshishi, Kitimu na Rodanimu.

*Wana Wa Hamu*

8 [e]Wana wa Hamu walikuwa:
Kushi, Misraimu,[f] Putu na Kanaani.
9 Wana wa Kushi walikuwa:
Seba, Havila, Sabta, Raama na Sabteka.
Wana wa Raama walikuwa:
Sheba na Dedani.
10 [g]Kushi akamzaa
Nimrodi, ambaye alikua akawa mtu shujaa katika nchi.
11 Misraimu akawazaa:
Waludi, Waanami, Walehabi,
Wanaftuhi, 12 [h]Wapathrusi,
Wakasluhi (hao ndio asili ya Wafilisti) na Wakaftori.
13 Wana wa Kanaani walikuwa:
Sidoni, mzaliwa wake wa kwanza,
na Hethi, 14 Wayebusi, Waamori,
Wagirgashi, 15 Wahivi, Waariki,
Wasini, 16 Waarvadi, Wasemari na
Wahamathi.

*Wana Wa Shemu*

17 [i]Wana wa Shemu walikuwa:
Elamu, Ashuru, Arfaksadi, Ludi na Aramu.
Wana wa Aramu walikuwa:
Usi, Huli, Getheri na Mesheki.
18 Arfaksadi akamzaa Shela,
Shela akamzaa Eberi.
19 Eberi alipata wana wawili:
Mmoja wao aliitwa Pelegi,[j] kwa kuwa wakati wake dunia iligawanyika; nduguye aliitwa Yoktani.
20 Wana wa Yoktani walikuwa:
Almodadi, Shelefu, Hasarmawethi,
Yera, 21 Hadoramu, Uzali, Dikla,
22 Obali, Abimaeli, Sheba, 23 Ofiri,
Havila na Yobabu. Wote hawa walikuwa wana wa Yoktani.

24 [k]Wana wa Shemu walikuwa
Arfaksadi, Shela,
25 [l]Eberi, Pelegi, Reu,
26 Serugi, Nahori, Tera,
27 [m]Tera akamzaa Abramu (yaani, Abrahamu).

*Jamaa Ya Abrahamu*

28 [n]Abrahamu alikuwa na wana wawili:
Isaki na Ishmaeli.

---

[a]**1:1** Mwa 5:1-32; Lk 3:36-38
[b]**1:2** Mwa 5:9; 5:12; 5:15
[c]**1:3** Mwa 5:18; Yud 14; Mwa 5:21; 5:25; 5:29
[d]**1:4** Mwa 6:10; 10:1; 5:32
[e]**1:8** Mwa 16:10
[f]8 Yaani Misri.
[g]**1:10** Mwa 10:8, 13
[h]**1:12** Mwa 10:14; Kum 2:23; Yer 47:4; Amo 9:7
[i]**1:17** Mwa 9:23-26; 10:22; 11:10
[j]19 Pelegi maana yake Mgawanyiko.
[k]**1:24** Mwa 10:21-29; Lk 3:34-36
[l]**1:25** Mwa 11:15; Hes 24:24; Lk 3:35
[m]**1:27** Mwa 17:5; 2Nya 20:7; Isa 41:8; 51:2; Rum 4:16
[n]**1:28** Mwa 21:2-3; 16:11, 15

*Wazao Wa Hagari*

**(Mwanzo 25:12-16)**

29 [a]Hawa ndio waliokuwa wazao wa Hagari:
Nebayothi mzaliwa wa kwanza wa Ishmaeli, Kedari, Adbeeli, Mibsamu, 30 Mishma, Duma, Masa, Hadadi, Tema, 31 Yeturi, Nafishi na Kedema. Hao ndio wana wa Ishmaeli.

*Wazao Wa Ketura*

32 [b]Wana waliozaliwa na Ketura suria wa Abrahamu walikuwa:
Zimrani, Yokshani, Medani, Midiani, Ishbaki na Shua.
Wana wa Yokshani walikuwa:
Sheba na Dedani.
33 Wana wa Midiani walikuwa:
Efa, Eferi, Hanoki, Abida na Eldaa.
Wote hao walikuwa wa uzao wa Ketura.

*Wazao Wa Sara*

34 [c]Abrahamu alikuwa baba wa Isaki.
Wana wa Isaki walikuwa:
Esau na Israeli.

*Wana Wa Esau*

**(Mwanzo 36:1-19)**

35 [d]Wana wa Esau walikuwa:
Elifazi, Reueli, Yeushi, Yalamu na Kora.
36 [e]Wana wa Elifazi walikuwa:
Temani, Omari, Sefo, Gatamu na Kenazi;
Elifazi kwa Timna akamzaa Amaleki.
37 [f]Wana wa Reueli walikuwa:
Nahathi, Zera, Shama na Miza.

*Watu Wa Seiri Waliokuwa Edomu*

**(Mwanzo 36:20-30)**

38 [g]Wana wa Seiri walikuwa:
Lotani, Shobali, Sibeoni, Ana, Dishoni, Eseri na Dishani.
39 [h]Wana wa Lotani walikuwa wawili:
Hori na Homamu. Lotani alikuwa na dada yake aliyeitwa Timna.
40 [i]Wana wa Shobali walikuwa:
Alvani,[j] Manahathi, Ebali, Shefo na Onamu.
Wana wa Sibeoni walikuwa:
Aiya na Ana.
41 [k]Mwana wa Ana alikuwa:
Dishoni.
Nao wana wa Dishoni walikuwa:
Hemdani, Eshbani, Ithrani na Kerani.
42 Wana wa Eseri walikuwa:
Bilhani, Zaavani na Akani.
Wana wa Dishani walikuwa:
Usi na Arani.

*Watawala Wa Edomu*

**(Mwanzo 36:31-43)**

43 [l]Hawa ndio wafalme waliotawala Edomu kabla hajatawala mfalme yeyote wa Waisraeli:
Bela mwana wa Beori, ambaye mji wake ni Dinhaba.
44 Bela alipofariki, Yobabu mwana wa Zera kutoka Bosra akawa mfalme baada yake.
45 [m]Yobabu alipofariki, Hushamu kutoka nchi ya Watemani akawa mfalme baada yake.
46 [n]Hushamu alipofariki, Hadadi mwana wa Bedadi, aliyeshinda Midiani katika nchi ya Moabu, akawa mfalme baada yake. Mji wake uliitwa Avithi.
47 Hadadi alipofariki, Samla kutoka

---

[a]**1:29** Mwa 25:13-26
[b]**1:32** Mwa 22:24; 10:7
[c]**1:34** Lk 3:34; Mwa 21:2-3; Mdo 7:8; Mwa 18:5; 25:25-26
[d]**1:35** Mwa 36:19; 36:4; Kum 2:22; Rum 9:13; Ebr 12:16; Mal 1:2-3
[e]**1:36** Kut 17:14; Mwa 36:11
[f]**1:37** Mwa 36:17
[g]**1:38** Mwa 36:20
[h]**1:39** Mwa 36:22
[i]**1:40** Mwa 36:2
[j]40 Maandishi ya Kiebrania yanamwita Alian.
[k]**1:41** Mwa 36:25-26
[l]**1:43** Mwa 36:31; 49:10
[m]**1:45** Mwa 36:11
[n]**1:46** 1Fal 11:14

Masreka akawa mfalme baada yake.
48 [a]Samla alipofariki, Shauli kutoka Rehobothi ng'ambo ya Mto Frati, akawa mfalme baada yake.
49 Shauli alipofariki, Baal-Hanani mwana wa Akbori akawa mfalme baada yake.
50 [b]Baal-Hanani alipofariki, Hadadi akawa mfalme baada yake. Mji wake uliitwa Pau, na mkewe aliitwa Mehetabeli binti Matredi,
binti Me-Zahabu. 51 [c]Naye Hadadi
pia akafa.

Wakuu wa Edomu walikuwa:
Timna, Alva, Yethethi,
52 Oholibama, Ela, Pinoni,
53 Kenazi, Temani, Mibsari,
54 Magdieli na Iramu. Hao ndio wakuu wa makabila ya Edomu.

## *Wana Wa Israeli*

2 [d]Hawa ndio waliokuwa wana wa Israeli:
Reubeni, Simeoni, Lawi, Yuda,
Isakari, Zabuloni, 2 Dani, Yosefu,
Benyamini, Naftali, Gadi na Asheri.

## *Yuda*

### *Hadi Wana Wa Hesroni*

3 [e]Wana wa Yuda walikuwa:
Eri, Onani na Shela. Hawa watatu walizaliwa kwake na mkewe Mkanaani, binti wa Shua. Eri, mzaliwa wa kwanza wa Yuda, alikuwa mwovu machoni pa Bwana, kwa hiyo Bwana
alimuua. 4 [f]Tamari, mkwewe Yuda,
alimzalia wana wawili: Peresi na Zera. Yuda alikuwa na jumla ya wana watano.

5 [g]Wana wa Peresi walikuwa:
Hesroni na Hamuli.
6 [h]Wana wa Zera walikuwa:
Zimri, Ethani, Hemani, Kalkoli na Dara. Jumla ya wana wa Zera walikuwa watano.
7 [i]Mwana wa Karmi alikuwa:
Akari,[j] ambaye alileta taabu kwa Waisraeli kwa kukiuka onyo la kutokuchukua vitu vilivyokuwa vimewekwa wakfu.
8 Mwana wa Ethani alikuwa:
Azariya.
9 [k]Wana wa Hesroni walikuwa:
Yerameeli, Ramu na Kalebu.

### *Kuanzia Ramu Mwana Wa Hesroni*

10 [l]Ramu alimzaa
Aminadabu, na Aminadabu akamzaa Nashoni, kiongozi
wa kabila la Yuda. 11 Nashoni
akamzaa Salmoni, Salmoni
akamzaa Boazi, 12 [m]Boazi akamzaa
Obedi, Obedi akamzaa Yese.
13 [n]Yese akawazaa
Eliabu mwanawe wa kwanza; wa pili Abinadabu, wa tatu Shimea,[o]
14 wa nne Nethaneli, wa tano
Radai, 15 wa sita Osemu, na wa
saba Daudi. 16 [p]Dada zao walikuwa
Seruya na Abigaili. Wana wa Seruya walikuwa watatu: Abishai,
Yoabu na Asaheli. 17 [q]Abigaili
alikuwa mama yake Amasa, ambaye baba yake alikuwa Yetheri, Mwishmaeli.

---

[a]**1:48** Mwa 36:37
[b]**1:50** Mwa 36:39
[c]**1:51** Mwa 36:40; Kut 15:15
[d]**2:1** Mwa 32:28; 35:10; Kut 32:13; Hes 1:5-15; 13:4-15; Mwa 29:32; 1Fal 18:31
[e]**2:3** Mwa 29:35; 38:2; Hes 26:19
[f]**2:4** Mwa 38:11-30; 11:31; 38:29
[g]**2:5** Mwa 46:12; Hes 26:21; Rut 4:18
[h]**2:6** 1Fal 4:31
[i]**2:7** Yos 7:1; 6:18; 1Nya 4:1
[j]7 Akari maana yake Taabisha; pia anaitwa Akani (Yos 6:1-26; 22:20).
[k]**2:9** Hes 26:21
[l]**2:10** Lk 3:32-33; Kut 6:23; Hes 1:7; Rut 4:19
[m]**2:12** Rut 2:1; 4:17
[n]**2:13** Rut 4:17; Isa 16:6
[o]13 Au: Shima, maana yake Sifa njema (pia 1Sam 16:9; 17:13).
[p]**2:16** 1Sam 26:6; 2Sam 2:18; 2:13
[q]**2:17** 2Sam 17:25

### *Kalebu Mwana Wa Hesroni*

18 Kalebu mwana wa Hesroni akazaa
wana na mkewe Azuba (na pia
na Yeriothi). Hawa ndio wana
Azuba aliomzalia Kalebu: Yesheri,
Shobabu na Ardoni. 19 [a]Azuba
alipofariki, Kalebu akamwoa
Efrathi, ambaye alimzalia Huri.
20 [b]Huri akamzaa Uri, Uri akamzaa
Bezaleli.

21 [c]Hatimaye, Hesroni akakutana
kimwili na binti wa Makiri
babaye Gileadi (ambaye alimwoa
alipokuwa na umri wa miaka
sitini), naye akamzaa Segubu.
22 Segubu akamzaa Yairi, ambaye
alitawala miji ishirini na mitatu
katika Gileadi. 23 [d](Lakini Geshuri
na Aramu wakateka miji ya
Hawoth-Yairi, pamoja na Kenathi
na viunga vyake; jumla ilikuwa
miji sitini.) Wote hawa walikuwa
wazao wa Makiri babaye Gileadi.

24 [e]Baada ya Hesroni kufa huko
Efrathi, Abiya mjane wa Hesroni
akamzalia Ashuru, aliye baba wa
Tekoa.

### *Yerameeli Mwana Wa Hesroni*

25 Wana wa Yerameeli mzaliwa wa
kwanza wa Hesroni walikuwa:
Ramu mzaliwa wake wa kwanza,
Buna, Oreni, Osemu na Ahiya.
26 Yerameeli alikuwa na mke
mwingine, aliyeitwa Atara,
aliyekuwa mama yake Onamu.

27 Wana wa Ramu mzaliwa wa kwanza
wa Yerameeli walikuwa:
Maasi, Yamini na Ekeri.

28 Wana wa Onamu walikuwa:
Shamai na Yada.
Wana wa Shamai walikuwa:
Nadabu na Abishuri.

29 Mke wa Abishuri aliitwa Abihaili,
ambaye alimzalia Abani na Molidi.

30 Wana wa Nadabu walikuwa
Seledi na Apaimu, lakini Seledi
alikufa bila kuzaa watoto.

31 Apaimu akamzaa:
Ishi ambaye alikuwa baba wa
Sheshani.
Sheshani akamzaa Alai.

32 Wana wa Yada, nduguye Shamai
walikuwa:
Yetheri na Yonathani. Yetheri
alikufa bila kuzaa watoto.

33 Wana wa Yonathani walikuwa:
Pelethi na Zaza.
Hawa ndio waliokuwa wazao wa
Yerameeli.

34 Sheshani hakuwa na watoto wa
kiume, ila wasichana tu.
Alikuwa na mtumishi Mmisri
aliyeitwa Yarha. 35 Sheshani
akamwoza huyu mtumishi wake
Yarha binti yake, akamzalia
mwana jina lake Atai.

36 [f]Atai akamzaa Nathani,
Nathani akamzaa Zabadi,
37 Zabadi akamzaa Eflali,
Eflali akamzaa Obedi,
38 Obedi akamzaa Yehu,
Yehu akamzaa Azaria,
39 Azaria akamzaa Helesi,
Helesi akamzaa Eleasa,
40 Eleasa akamzaa Sismai,
Sismai akamzaa Shalumu,
41 Shalumu akamzaa Yekamia,
naye Yekamia akamzaa Elishama.

### *Koo Za Kalebu*

42 Wana wa Kalebu nduguye Yerameeli
walikuwa:
Mesha mzaliwa wake wa kwanza
alimzaa Zifu, naye mwanawe
Maresha akamzaa Hebroni.

43 Hebroni alikuwa na wana wanne:
Kora, Tapua, Rekemu na Shema.
44 Shema alikuwa baba yake
Rahamu na Rahamu alikuwa baba
wa Yorkeamu na Rekemu alikuwa

---

[a]**2:19** 1Nya 2:42, 50
[b]**2:20** Kut 32:2; 35:30; 2Nya 1:5
[c]**2:21** Hes 21:1
[d]**2:23** Hes 32:41; 32:42; Yos 13:30; Kum 3:14
[e]**2:24** 1Nya 4:5; 2Nya 11:6; 20:20; 2Sam 14:2; Neh 3:5; Yer 6:1
[f]**2:36** 1Nya 11:41

baba wa Shamai. 45 [a]Shamai
akamzaa Maoni na Maoni
akamzaa Beth-Suri.
46 Efa, suria wa Kalebu alikuwa
mamaye Harani, Mosa na Gazezi.
Harani alikuwa baba wa Gazezi.
47 Wana wa Yadai walikuwa:
Regemu, Yothamu, Geshani,
Peleti, Efa na Shaafu.
48 Maaka suria wa Kalebu alikuwa
mamaye Sheberi na Tirhana.
49 [b]Pia Maaka akamzaa Shaafu
babaye Madmana, na Sheva
babaye Makbena na Gibea. Kalebu
alikuwa na binti jina lake Aksa.
50 [c]Hawa ndio waliokuwa wazao
wa Kalebu.

Wana wa Huri, mzaliwa mkuu wao
wa Efrathi, walikuwa:
Shobali akamzaa Kiriath-Yearimu,
51 Salma akamzaa Bethlehemu,
naye Harefu akamzaa Beth-Gaderi.
52 Wazao wa Shobali, baba yake
Kiriath-Yearimu, walikuwa:
Haroe, nusu ya wakazi wa mji
wa Menuhothi, 53 [d]pamoja na koo
za Kiriath-Yearimu ambazo ni:
Waithiri, Waputhi, Washumathi
na Wamishrai. Kutokana na watu
hawa walizaliwa Wasorathi na
Waeshtaoli.
54 [e]Wazao wa Salma walikuwa:
Bethlehemu, Wanetofathi,
Atroth-Beth-Yoabu, nusu ya
Wamanahathi, Wasori, 55 [f]pamoja
na koo za waandishi zilizoishi
katika mji wa Yabesi: yaani
Watirathi, Washimeathi na
Wasukathi. Hawa ndio Wakeni
waliotokana na Hamathi, baba wa
nyumba ya Rekabu.

[a]**2:45** Yos 15:55; 15:58
[b]**2:49** Yos 15:31; 15:16
[c]**2:50** 1Nya 4:4; 2:19
[d]**2:53** 2Sam 23:38
[e]**2:54** Ezr 2:22; Neh 12:28
[f]**2:55** Mwa 15:19; Amu 1:16; Yos 19:35; 2Fal 10:15, 23; Yer 35:2-19; Amu 4:11; Hes 24:21-22

*Wana Wa Daudi*

3 [g]Hawa ndio waliokuwa wana wa
Daudi waliozaliwa huko Hebroni:
Mzaliwa wa kwanza alikuwa
Amnoni ambaye mama yake
aliitwa Ahinoamu wa Yezreeli;
wa pili, Danieli ambaye mama
yake alikuwa Abigaili wa Karmeli;
2 [h]wa tatu alikuwa Absalomu,
ambaye mama yake alikuwa
Maaka, binti Talmai mfalme wa
Geshuri;
wa nne, Adoniya, ambaye mama
yake alikuwa Hagithi;
3 [i]wa tano alikuwa Shefatia ambaye
mama yake alikuwa Abitali;
wa sita alikuwa Ithreamu,
aliyezaliwa na mke wake Egla.
4 [j]Hawa sita walizaliwa huko
Hebroni ambako Daudi alitawala
kwa miaka saba na miezi sita.

Daudi alitawala Yerusalemu kwa miaka
thelathini na mitatu, 5 [k]nao hawa ndio
watoto wa Daudi waliozaliwa huko
Yerusalemu:

mkewe Bathsheba, binti Amieli,
alimzalia Shamua,[l] Shobabu,
Nathani na Solomoni. 6 Pia
kulikuwa na wana wengine:
Ibihari, Elishua, Elifeleti, 7 Noga,
Nefegi, Yafia, 8 [m]Elishama, Eliada
na Elifeleti; wote walikuwa tisa.
9 [n]Hawa wote walikuwa wana
wa Daudi, mbali na wale wana
waliozaliwa na masuria. Naye
Tamari alikuwa dada yao.

[g]**3:1** 1Nya 14:3; 14:3; 28:5; Yos 15:56; 1Sam 25:42; 27:3
[h]**3:2** 1Fal 2:22
[i]**3:3** 2Sam 3:5
[j]**3:4** 2Sam 5:4; 1Nya 29:27; 1Sam 2:11; 5:5; 1Fal 2:11
[k]**3:5** 2Sam 11:3; 12:24; 1Nya 14:4
[l]5 Sawa na Shimea; maana yake ni Mashuhuri, Maarufu.
[m]**3:8** 2Sam 5:14
[n]**3:9** 2Sam 13:1; 1Nya 14:4; 2Sam 14:27

*Wafalme Wa Yuda*

10 [a]Mwana wa Solomoni alikuwa
Rehoboamu,
mwanawe huyo alikuwa Abiya,
mwanawe huyo alikuwa
Yehoshafati,
mwanawe huyo alikuwa Asa,
11 [b]mwanawe huyo alikuwa
Yehoramu,
mwanawe huyo alikuwa Ahazia,
mwanawe huyo alikuwa Yoashi,
12 [c]mwanawe huyo alikuwa Amazia,
mwanawe huyo alikuwa Azaria,
mwanawe huyo alikuwa Yothamu,
13 mwanawe huyo alikuwa Ahazi,
mwanawe huyo alikuwa Hezekia,
mwanawe huyo alikuwa Manase,
14 mwanawe huyo alikuwa Amoni
na mwanawe huyo alikuwa Yosia.
15 [d]Wana wa Yosia walikuwa:
Yohanani mzaliwa wake wa
kwanza,
Yehoyakimu mwanawe wa pili,
wa tatu Sedekia,
wa nne Shalumu.
16 [e]Walioingia mahali pa Yehoyakimu
kama wafalme ni:
Yekonia mwanawe,
na Sedekia.

*Ukoo Wa Kifalme Baada Ya Uhamisho*

17 [f]Hawa ndio waliokuwa wazao wa
Yekonia aliyekuwa mateka:
Shealtieli mwanawe,
18 [g]Malkiramu, Pedaya, Shenasari,
Yekamia, Hoshama na Nedabia.
19 [h]Wana wa Pedaya walikuwa:
Zerubabeli na Shimei.
Wana wa Zerubabeli walikuwa:
Meshulamu na Hanania.
Shelomithi alikuwa dada yao.
20 Pia walikuwepo wengine watano:
Hashuba, Oheli, Berekia, Hasadia
na Yushab-Hesedi.
21 Wazao wa Hanania walikuwa:
Pelatia na Yeshaya, na wana wa
Refaya, na wana wa Arnani, na
wana wa Obadia, na wana wa
Shekania.
22 [i]Wazao wa Shekania:
Shemaya na wanawe:
Hatushi, Igali, Baria, Nearia na
Shafati; jumla yao walikuwa sita.
23 Wana wa Nearia walikuwa:
Elioenai, Hizkia na Azrikamu;
jumla yao watatu.
24 Wana wa Elioenai walikuwa:
Hodavia, Eliashibu, Pelaya,
Akubu, Yohanani, Delaya na
Anani; jumla yao wote saba.

*Koo Nyingine Za Yuda*

4 [j]Wana wa Yuda walikuwa:
Peresi, Hesroni, Karmi, Huri na
Shobali.
2 Reaya mwana wa Shobali akamzaa
Yahathi, Yahathi akawazaa
Ahumai na Lahadi. Hizi ndizo
zilizokuwa koo za Wasorathi.
3 Hawa ndio waliokuwa wana wa
Etamu:
Yezreeli, Ishma na Idbashi. Dada
yao aliitwa Haselelponi. 4 [k]Penueli
akamzaa Gedori, naye Ezeri
akamzaa Husha.
Hawa walikuwa wazao wa Huri,
mzaliwa wa kwanza wa Efrathi, na
baba yake Bethlehemu.
5 [l]Ashuri baba yake Tekoa alikuwa na
wake wawili, Hela na Naara.
6 Hawa walikuwa wazao wa Naara:
Ahuzamu, Heferi, Temeni na
Haahashtari.
7 Wana wa Hela walikuwa:

[a] **3:10** 1Fal 14:21-31; 15:1-8; 2Nya 12:16; 13:1; 17:1–21:3
[b] **3:11** 2Fal 8:16-24; 2Nya 21:1; 22:1-10; 2Fal 11:1-12
[c] **3:12** 2Fal 14:1-22; 2Nya 25:1-28; 27:1; Isa 1:1; 3:13; 2Nya 28:1; Isa 1:1; 2Fal 21:1-18; 2Nya 33:1
[d] **3:15** 2Fal 23:34; Yer 37:1; 2Fal 25:3
[e] **3:16** 2Fal 24:6, 8; Mt 1:11; 2Fal 24:18
[f] **3:17** Ezr 3:2
[g] **3:18** Ezr 1:8; 5:14; Yer 22:30
[h] **3:19** Hag 2:2; Zek 4:6; Ezr 3:2
[i] **3:22** Ezr 8:2-3
[j] **4:1** Mwa 46:12; 1Nya 2:3; Hes 26:21; Mwa 38:29; Rut 4:18
[k] **4:4** 1Nya 2:50; Rut 1:19
[l] **4:5** 1Nya 2:24

Serethi, Sohari, Ethnani, [8] na Kosi
ambaye aliwazaa Anubi, Sobeba
na jamaa zote za Aharheli mwana
wa Harumu.

9 [a]Yabesi aliheshimiwa kuliko ndugu
zake. Mama yake alimwita Yabesi, akisema,
“Nilimzaa kwa huzuni.” 10 [b]Yabesi akamlilia
Mungu wa Israeli akisema, “Ee Mungu,
laiti ungenibariki kweli kweli na kuipanua
mipaka yangu! Mkono wako na uwe pamoja
nami, uniepushe na uovu ili nisidhurike!”
Naye Mungu akamjalia hayo aliyoyaomba.

11 Kelubu, nduguye Shuha, akamzaa
Mehiri, naye Mehiri akamzaa
Eshtoni. 12 Eshtoni akawazaa Beth-
Rafa, Pasea na Tehina. Tehina
alikuwa baba wa Iri-Nahashi.
Hawa ndio waliokuwa wazao wa
Reka.

13 [c]Wana wa Kenazi walikuwa:
Othnieli na Seraya.
Wana wa Othnieli walikuwa:
Hathathi na Meonathai.
14 [d]Meonathai akamzaa Ofra.
Seraya akamzaa Yoabu,
baba wa Ge-Harashimu.[e] Liliitwa
hivyo kwa sababu watu walioishi
humo walikuwa mafundi.
15 Kalebu mwana wa Yefune alikuwa
na wana watatu:
Iru, Ela na Naamu.
Naye mwana wa Ela alikuwa:
Kenazi.
16 Wana wa Yahaleleli walikuwa:
Zifu, Zifa, Tiria na Asareli.
17 [f]Wana wa Ezra walikuwa:
Yetheri, Meredi, Eferi na Yaloni.
Mmojawapo wa wake zake Meredi
aliwazaa: Miriamu, Shamai
na Ishba aliyekuwa baba yake
Eshtemoa. 18 [g]Meredi alikuwa
na mke mwingine Myahudi
ambaye aliwazaa: Yeredi baba wa
Gedori, Heberi baba wa Soko na
Yekuthieli baba wa Zanoa. Hawa
walikuwa watoto wa Bithia binti
Farao, ambaye Meredi alikuwa
amemwoa.
19 [h]Wana wa mke wa Hodia aliyekuwa
dada yake Nahamu walikuwa:
baba yake Keila, Mgarmi na
Eshtemoa, Mmaakathi.
20 Wana wa Shimoni walikuwa:
Amnoni, Rina, Ben-Hanani na
Tiloni.
Wazao wa Ishi walikuwa:
Zohethi na Ben-Zohethi.
21 [i]Wana wa Shela, mwana wa Yuda,
walikuwa:
Eri baba yake Leka, Laada
baba yake Maresha na jamaa
za wafumaji nguo za kitani
safi waliokuwa wakiishi huko
Beth-Ashbea, 22 [j]Yokimu, watu
walioishi Kozeba, Yoashi na
Sarafi waliotawala huko Moabu
na Yashubi-Lehemu. (Taarifa
hizi ni za zamani sana.) 23 Hawa
walikuwa wafinyanzi walioishi
Netaimu na Gedera; waliishi huko
wakimtumikia mfalme.

*Simeoni*

24 [k]Wazao wa Simeoni walikuwa:
Nemueli, Yamini, Yaribu, Zera na
Shauli.
25 Mwana wa Shauli alikuwa
Shalumu, Shalumu akamzaa
Mibsamu, na Mibsamu akamzaa
Mishma.
26 Wazao wa Mishma walikuwa:
Hamueli aliyemzaa Zakuri, Zakuri
akamzaa Shimei.

27 Shimei alikuwa na wana kumi na sita,

---

[a]**4:9** Mwa 34:19; Za 112:6; Mit 10:7; Mwa 3:16
[b]**4:10** Mwa 12:8; 1Nya 16:8; Ay 12:4; 22:27; Isa 12:4; 1Fal 3:7-13; Mt 7:7-11; Za 21:4; 65:2
[c]**4:13** Yos 15:17
[d]**4:14** Neh 11:35
[e]14 Maana yake Bonde la Mafundi.
[f]**4:17** Kut 15:20
[g]**4:18** Yos 15:34
[h]**4:19** Yos 15:44; Kum 3:14
[i]**4:21** Mwa 38:5
[j]**4:22** 2Sam 8:2
[k]**4:24** Mwa 21:14; Yos 15:26

na binti sita, lakini ndugu zake hawakuwa
na watoto wengi, hivyo ukoo wao wote
haukuwa na watu wengi kama ukoo wa
Yuda. 28 Waliishi Beer-Sheba, Molada, Hasar-
Shuali, 29 [a]Bilha, Esemu, Toladi, 30 Bethueli,
Horma, Siklagi, 31 [b]Beth-Markabothi, Hasar-
Susimu, Beth-Biri na Shaaraimu. Hii ilikuwa
miji yao mpaka wakati wa utawala wa
Daudi. 32 [c]Vijiji vilivyoizunguka vilikuwa
Etamu, Aini, Rimoni, Tokeni na Ashani;
jumla miji mitano: 33 pamoja na vijiji
vyote kuizunguka hii miji hadi huko Baali.
Haya yalikuwa makao yao, nao waliweka
kumbukumbu ya ukoo wao.

34 Meshobabu, Yamleki, Yosha mwana
wa Amazia, 35 Yoeli, Yehu mwana wa
Yoshibia, mwana wa Seraya, mwana
wa Asieli. 36 Pia Elioenai, Yaakoba,
Yeshohaya, Asaya, Adieli, Yesimieli,
Benaya, 37 Ziza mwana wa Shifi, mwana
wa Aloni, mwana wa Yedaya, mwana
wa Shimri, mwana wa Shemaya.

38 Watu hawa walioorodheshwa hapa juu
kwa majina walikuwa viongozi wa koo zao.
Jamaa zao ziliongezeka sana, 39 [d]wakaenea
mpaka kwenye viunga vya Gedori kuelekea
mashariki mwa bonde wakitafuta malisho
kwa ajili ya mifugo yao. 40 [e]Huko walipata
malisho mengi mazuri, nayo nchi ilikuwa
na nafasi kubwa, yenye amani na utulivu.
Baadhi ya Wahamu waliishi huko zamani.
41 [f]Watu walioorodheshwa majina
walikuja katika nchi hiyo wakati wa
Hezekia mfalme wa Yuda. Akawashambulia
Wahamu katika makao yao pamoja na
Wameuni ambao walikuwako huko nao
wakawaangamiza kabisa, kama ilivyo
dhahiri hadi leo. Kisha wakafanya makazi
yao huko kwa sababu kulikuwa na malisho
mazuri kwa ajili ya mifugo yao. 42 [g]Watu wa
kabila la wa Simeoni wapatao mia tano,
wakiongozwa na Pelatia, Nearia, Refaya
na Uzieli wana wa Ishi, wakavamia nchi ya
vilima ya Seiri. 43 [h]Wakawaua Waamaleki
waliobaki, waliokuwa wamenusurika, nao
wanaishi huko hadi leo.

*Wana Wa Reubeni*

5 [i]Wana wa Reubeni mzaliwa wa kwanza
wa Israeli (yeye alikuwa mzaliwa wa
kwanza, lakini kwa kuwa alikinajisi kitanda
cha baba yake, haki zake za mzaliwa wa
kwanza walipewa wana wa Yosefu mwana
wa Israeli. Hivyo hakuorodheshwa kwenye
orodha ya ukoo wao kulingana na haki yake
ya kuzaliwa. 2 [j]Na ingawa Yuda alikuwa
na nguvu zaidi ya ndugu zake wote, na
mtawala alitoka kwake, haki za mzaliwa
wa kwanza zilikuwa za Yosefu.) 3 [k]Wana
wa Reubeni mzaliwa wa kwanza wa Israeli
walikuwa:

Hanoki, Palu, Hesroni na Karmi.
4 Wazao wa Yoeli walikuwa:
Shemaya mwanawe, Gogu
mwanawe;
Shimei mwanawe, 5 Mika
mwanawe,
Reaya mwanawe, Baali mwanawe,
6 [l]na Beera mwanawe, ambaye
Tiglath-Pileseri mfalme wa Ashuru
alimchukua kwenda uhamishoni.
Beera alikuwa kiongozi wa
Wareubeni.
7 [m]Jamaa zao kulingana na koo zao,
walioorodheshwa kwa kufuata koo
zao kama ifuatavyo:
Yeieli aliyekuwa mkuu wao,
Zekaria, 8 [n]Bela mwana wa Azazi,
mwana wa Shema, mwana wa
Yoeli. Hao waliishi katika eneo
kuanzia Aroeri mpaka Nebo na

[a]**4:29** Yos 15:29
[b]**4:31** Yos 15:35
[c]**4:32** Hes 34:11; Yos 15:42
[d]**4:39** Yos 15:58
[e]**4:40** Amu 18:7-10; Mwa 9:22; 10:6; Za 78:51
[f]**4:41** 2Nya 20:1; 26:7; 2Fal 18:8
[g]**4:42** Mwa 14:6
[h]**4:43** 1Sam 15:8; 2Sam 8:12
[i]**5:1** Mwa 29:32; 35:22; 49:4; 48:16; 49:26; 48:5; 1Nya 26:10
[j]**5:2** Mwa 49:10; 49:12; Za 60:7; Mt 2:6; Mwa 25:31; Hes 2:3; 7:12; Za 108:8; 78:68-71; Yer 23:5-6; Mik 5:2
[k]**5:3** Kut 6:19; Hes 26:5-11; 26:5; Mwa 46:9
[l]**5:6** 2Fal 16:10; 2Nya 28:20; 2Fal 15:29
[m]**5:7** Mit 17; Yos 13:17
[n]**5:8** Hes 32:34; Amu 11:26; Yos 13:17

Baal-Meoni. 9 [a]Kwa upande wa
mashariki walienea hadi pembeni
mwa jangwa linaloenea mpaka
kwenye Mto Frati, kwa sababu
mifugo yao ilikuwa imeongezeka
huko Gileadi.

10 [b]Wakati wa utawala wa Mfalme
Sauli, walipigana vita dhidi ya
Wahagari, wakaanguka kwa mikono
yao, kisha wakaishi katika mahema ya
Wahagari katika eneo lote la mashariki
ya Gileadi.

*Wana Wa Gadi*

11 [c]Wagadi waliishi jirani nao katika
nchi ya Bashani, mpaka Saleka.
12 Yoeli ndiye alikuwa mkuu wao,
Shafamu wa pili, na wakafuata
Yanai na Shafati, huko Bashani.
13 Ndugu zao kulingana na koo zao
walikuwa saba:
Mikaeli, Meshulamu, Sheba, Yorai,
Yakani, Zia na Eberi.
14 Hawa walikuwa ndio wana wa
Abihaili mwana wa Huri, mwana
wa Yaroa, mwana wa Gileadi,
mwana wa Mikaeli, mwana wa
Yeshishai, mwana wa Yahdo,
mwana wa Buzi.
15 Ahi mwana wa Abdieli, mwana wa
Guni, alikuwa ndiye kiongozi wa
jamaa yao.
16 [d]Wagadi waliishi Gileadi, huko
Bashani pamoja na vijiji
vilivyoizunguka, pia katika nchi
yote ya malisho ya Sharoni kote
walikoenea.

17 [e]Yote haya yaliwekwa katika
kumbukumbu za ukoo wao wakati wa
utawala wa Yothamu, mfalme wa Yuda na
Yeroboamu mfalme wa Israeli.

18 [f]Wareubeni, Wagadi na nusu ya kabila
la Manase walikuwa na watu mashujaa
44,760 waliokuwa wameandaliwa kwa
ajili ya vita: watu wenye nguvu, hodari
wa kutumia ngao na upanga, mashujaa
wa kutumia upinde, waliokuwa tayari
kwa ajili ya kazi hiyo. 19 [g]Walipigana vita
dhidi ya Wahagari, Yeturi, Nafishi na
Nodabu. 20 [h]Walisaidiwa katika kupigana
nao, Mungu akawatia Wahagari pamoja
na wote walioungana nao mikononi
mwao, kwa sababu walimlilia Mungu
wakati wa vita. Alijibu maombi yao, kwa
sababu walimtegemea. 21 Walitwaa mifugo
ya Wahagari: ngamia 50,000, kondoo
250,000, punda 2,000. Pia wakateka watu
100,000, 22 [i]na wengine wengi waliuawa
kwa sababu vita vilikuwa ni vya Mungu.
Nao waliendelea kuikalia nchi hiyo mpaka
wakati wa uhamisho.

*Nusu Ya Kabila La Manase*

23 [j]Idadi ya nusu ya kabila la Manase
walikuwa wengi sana, Wakakaa kuanzia
Bashani hadi Baal-Hermoni, yaani mpaka
Seniri na mlima Hermoni.

24 Hawa ndio waliokuwa viongozi wa
jamaa za kabila hilo: Eferi, Ishi, Elieli,
Azrieli, Yeremia, Hodavia na Yahdieli.
Walikuwa askari shujaa watu maarufu,
viongozi wa jamaa zao. 25 [k]Lakini hawakuwa
waaminifu kwa Mungu wa baba zao, nao
wakafanya ukahaba kwa miungu ya mataifa,
ambayo Mungu alikuwa ameyaangamiza
mbele yao. 26 [l]Kwa hiyo Mungu wa Israeli
akaiamsha roho ya Pulu, mfalme wa
Ashuru (ambaye pia alijulikana kama
Tiglath-Pileseri), ambaye aliwachukua
Wareubeni, Wagadi na nusu ya kabila la
Manase kwenda uhamishoni. Akawapeleka
huko Hala, Habori, Hara na mto Gozani,
ambako wamekaa mpaka leo.

---

[a]**5:9** Hes 32:26; Yos 22:9; Wim 4:1; Mik 7:14
[b]**5:10** Mwa 25:12
[c]**5:11** Mwa 30:11; Yos 13:24-28; Kum 3:10; Yos 13:11
[d]**5:16** Mit 18:21; 1Nya 27:31; Isa 35:2; 65:10
[e]**5:17** 2Fal 15:32; 14:23
[f]**5:18** Hes 1:3
[g]**5:19** Mwa 28:15; 1Nya 1:31; Mwa 25:15
[h]**5:20** Za 46:5; 54:4; 20:7-9; 2Nya 6:34; Isa 26:3; Dan 6:23; Za 9:10; Yer 17:7-8
[i]**5:22** Kum 20:4; 2Nya 32:8; 1Nya 5:10; 2Fal 15:29
[j]**5:23** Kum 3:8, 9; Wim 4:8
[k]**5:25** 2Fal 17:7; 2Nya 12:2; Kut 34; 15; Law 18:3; Yer 5:7; Kum 32:15
[l]**5:26** Isa 37:7; 2Fal 15:19; 15:29; 17:6; 18:11

*Wana Wa Lawi*

6 [a]Wana wa Lawi walikuwa:
Gershoni, Kohathi na Merari.
2 Wana wa Kohathi walikuwa:
Amramu, Ishari, Hebroni na
Uzieli.
3 [b]Amramu alikuwa na wana:
Aroni, Mose, na Miriamu.
Aroni alikuwa na wana:
Nadabu, Abihu, Eleazari na
Ithamari.
4 Eleazari akamzaa Finehasi,
Finehasi akamzaa Abishua,
5 Abishua akamzaa Buki,
Buki akamzaa Uzi,
6 Uzi akamzaa Zerahia,
Zerahia akamzaa Merayothi,
7 Merayothi akamzaa Amaria,
Amaria akamzaa Ahitubu,
8 [c]Ahitubu akamzaa Sadoki,
Sadoki akamzaa Ahimaasi,
9 Ahimaasi akamzaa Azaria,
Azaria akamzaa Yohanani,
10 [d]Yohanani akamzaa Azaria
(ndiye alifanya kazi ya ukuhani
katika Hekalu alilojenga Mfalme
Solomoni huko Yerusalemu),
11 [e]Azaria akamzaa Amaria,
Amaria akamzaa Ahitubu,
12 Ahitubu akamzaa Sadoki,
Sadoki akamzaa Shalumu,
13 [f]Shalumu akamzaa Hilkia,
Hilkia akamzaa Azaria,
14 [g]Azaria akamzaa Seraya,
Seraya akamzaa Yehosadaki.
15 [h]Yehosadaki alihamishwa wakati
BWANA aliwapeleka uhamishoni
watu wa Yuda na Yerusalemu kwa
mkono wa Mfalme Nebukadneza.

16 [i]Wana wa Lawi walikuwa:
Gershoni, Kohathi na Merari.

17 Haya ndiyo majina ya wana wa
Gershoni:
Libni na Shimei.
18 Wana wa Kohathi walikuwa:
Amramu, Ishari, Hebroni na
Uzieli.
19 [j]Wana wa Merari walikuwa:
Mahli na Mushi.

Zifuatazo ni koo za Walawi
zilizoorodheshwa kufuatana na
baba zao:
20 Wazao wa Gershoni:
Gershoni akamzaa Libni, Libni
akamzaa Yahathi,
Yahathi akamzaa Zima, 21 [k]Zima
akamzaa Yoa,
Yoa akamzaa Ido, Ido akamzaa
Zera,
Zera akamzaa Yeatherai.
22 [l]Wazao wa Kohathi:
Kohathi akamzaa Aminadabu,
Aminadabu akamzaa Kora,
Kora akamzaa Asiri, 23 Asiri
akamzaa Elikana,
Elikana akamzaa Ebiasafu,
Ebiasafu akamzaa Asiri,
24 [m]Asiri akamzaa Tahathi, Tahathi
akamzaa Urieli,
Urieli akamzaa Uzia, Uzia
akamzaa Shauli.
25 Wazao wa Elikana walikuwa:
Amasai na Ahimothi,
26 Ahimothi akamzaa Elikana,
Elikana akamzaa Sofai,
Sofai akamzaa Nahathi, 27 [n]Nahathi
akamzaa Eliabu,
Eliabu akamzaa Yerohamu,
Yerohamu akamzaa Elikana,
Elikana akamzaa Samweli.
28 [o]Wana wa Samweli walikuwa:
Yoeli mzaliwa wake wa kwanza,
na Abiya mwanawe wa pili.
29 Wafuatao ndio wazao wa Merari:

---

[a]**6:1** Mwa 29:34; Kut 6:16
[b]**6:3** Law 10:1–20:2; Kut 6:23; 24:1
[c]**6:8** 2Sam 15:27; Ezr 7:2; 2Sam 8:17
[d]**6:10** 1Fal 6:1; 2Nya 3:1; 26:17-18
[e]**6:11** Ezr 7:3
[f]**6:13** 2Fal 22:5-20; 2Nya 35:8
[g]**6:14** Ezr 2:2; Neh 11:11
[h]**6:15** 2Fal 25:18; Zek 6:11; 2Nya 36:17-21
[i]**6:16** Mwa 29:34; Kut 6:16; Hes 26:57
[j]**6:19** Mwa 46:11; 1Nya 23:21; Hes 3:33
[k]**6:21** 1Nya 6:41-42
[l]**6:22** Kut 6:24
[m]**6:24** 1Nya 15:5
[n]**6:27** 1Sam 1:1; 1:20
[o]**6:28** 1Nya 6:33; 1Sam 8:2

Merari akamzaa Mahli, Mahli akamzaa Libni,
Libni akamzaa Shimei, Shimei akamzaa Uza,
30 Uza akamzaa Shimea, Shimea akamzaa Hagia,
Hagia akamzaa Asaya.

*Waimbaji Wa Hekalu*

31 [a]Hawa ndio watu ambao Daudi aliwaweka kuwa viongozi wa uimbaji katika nyumba ya BWANA, baada ya Sanduku la Agano kuletwa ili kukaa
huko. 32 Walihudumu kwa kuimba mbele ya Maskani, Hema la Kukutania, mpaka hapo Mfalme Solomoni alipojenga Hekalu la BWANA huko Yerusalemu. Walitimiza wajibu wao kulingana na taratibu walizokuwa wamewekewa.
33 [b]Wafuatao ni watu waliohudumu pamoja na wana wao:

Kutoka ukoo wa Kohathi walikuwa:
Hemani, mpiga kinanda,
alikuwa mwana wa Yoeli, mwana wa Samweli,
34 [c]mwana wa Elikana, mwana wa Yerohamu,
mwana wa Elieli, mwana wa Toa,
35 mwana wa Sufu, mwana wa Elikana,
mwana wa Mahathi, mwana wa Amasai,
36 mwana wa Elikana, mwana wa Yoeli,
mwana wa Azaria, mwana wa Sefania,
37 [d]mwana wa Tahathi, mwana wa Asiri,
mwana wa Ebiasafu, mwana wa Kora,
38 [e]mwana wa Ishari, mwana wa Kohathi,
mwana wa Lawi, mwana wa Israeli;
39 [f]na msaidizi wa Hemani alikuwa Asafu, aliyesimama mkono wa kuume:
Asafu mwana wa Berekia, mwana wa Shimea,
40 mwana wa Mikaeli, mwana wa Baaseya,
mwana wa Malkiya, 41 mwana wa Ethni,
mwana wa Zera, mwana wa Adaya,
42 mwana wa Ethani, mwana wa Zima,
mwana wa Shimei, 43 mwana wa Yahathi,
mwana wa Gershoni, mwana wa Lawi.
44 Na kutoka kwa walioshirikiana nao, Wamerari, mkono wake wa kushoto:
Ethani mwana wa Kishi, mwana wa Abdi,
mwana wa Maluki, 45 mwana wa Hashabia,
mwana wa Amazia, mwana wa Hilkia,
46 mwana wa Amsi, mwana wa Bani,
mwana wa Shemeri, 47 mwana wa Mahli,
mwana wa Mushi, mwana wa Merari,
mwana wa Lawi.

48 [g]Ndugu zao wengine Walawi walipewa huduma nyingine za kuhudumia hema
takatifu, nyumba ya Mungu. 49 [h]Lakini Aroni na uzao wake ndio waliokuwa na wajibu wa kutoa sadaka katika madhabahu ya sadaka ya kuteketezwa na kwenye madhabahu ya kufukizia uvumba pamoja na yote yaliyofanyika pa Patakatifu, wakifanya upatanisho kwa ajili ya Israeli, sawasawa na yale yote aliyoagiza Mose mtumishi wa Mungu.

[a]**6:31** 2Nya 29:25-26; Neh 12:45; Ezr 3:10; Za 68:29; 1Nya 16:1; 2Sam 6:17; 1Fal 8:4
[b]**6:33** 1Fal 4:31; 1Nya 15:17; Mit 28
[c]**6:34** 1Sam 1:1
[d]**6:37** Kut 6:24
[e]**6:38** Kut 6:21
[f]**6:39** 2Nya 29:13; Neh 11:17; 1Nya 15:17
[g]**6:48** 1Nya 23:32
[h]**6:49** Kut 27:1-8; 30:1-7, 10; 2Nya 26:18; Kut 29:38; Hes 3:10; 18:7; Ebr 5:1; 1Sam 2:28; 1Nya 23:13

50 [a]Hawa ndio waliokuwa wazao wa
Aroni:
Aroni akamzaa Eleazari, Eleazari
akamzaa Finehasi,
Finehasi akamzaa Abishua,
51 Abishua akamzaa Buki,
Buki akamzaa Uzi, Uzi akamzaa
Zerahia,
52 Zerahia akamzaa Merayothi,
Merayothi akamzaa Amaria,
Amaria akamzaa Ahitubu,
53 [b]Ahitubu akamzaa Sadoki,
Sadoki akamzaa Ahimaasi.

54 [c]Zifuatazo ni sehemu walizopewa ziwe
nchi yao kwa ajili ya makazi yao (walipewa
wazao wa Aroni waliotoka katika ukoo wa
Wakohathi, kwa sababu kura ya kwanza
iliwaangukia):

55 [d]Walipewa Hebroni katika nchi ya
Yuda pamoja na sehemu ya malisho
inayouzunguka. 56 [e]Lakini mashamba
pamoja na vijiji vilivyouzunguka mji
alipewa Kalebu mwana wa Yefune.
57 [f]Kwa hiyo wazao wa Aroni
walipewa miji ifuatayo pamoja na
eneo la malisho: Hebroni (mji wa
makimbilio), Libna, Yatiri, Eshtemoa,
58 [g]Hileni, Debiri, 59 [h]Ashani, Yuta na
Beth-Shemeshi pamoja na maeneo
yake ya malisho. 60 [i]Kutoka kabila la
Benyamini walipewa Gibeoni, Geba,
Alemethi na Anathothi, pamoja na
maeneo yake ya malisho.

Miji hii kumi na mitatu iligawanywa
miongoni mwa koo za Wakohathi.

61 Wazao waliobaki wa Wakohathi
walipewa miji kumi kutoka koo za nusu
ya kabila la Manase.
62 Wazao wa Gershoni, ukoo kwa ukoo,
walipewa miji kumi na mitatu kutoka kwa
makabila ya Isakari, Asheri na Naftali
kutoka sehemu ya kabila la Manase huko
Bashani.
63 [j]Wazao wa Merari, ukoo kwa ukoo
walipewa miji kumi na miwili kutoka
makabila ya Reubeni, Gadi na Zabuloni.
64 [k]Kwa hiyo Waisraeli waliwapa Walawi
miji hii pamoja na maeneo yake ya malisho.
65 Kutoka makabila ya Yuda, Simeoni na
Benyamini walipewa miji iliyotajwa hapo
juu.
66 Baadhi ya koo za Wakohathi walipewa
kama nchi yao miji kutoka kabila la
Efraimu.

67 [l]Katika nchi ya vilima ya
Efraimu walipewa Shekemu (mji wa
makimbilio) na Gezeri, 68 [m]Yokmeamu,
Beth-Horoni, 69 [n]Aiyaloni na Gath-
Rimoni, pamoja na maeneo yake ya
malisho.
70 Kutoka nusu ya kabila la Manase,
Waisraeli waliwapa koo za Wakohathi
waliobaki miji ya Aneri na Bileamu
pamoja na maeneo yake ya malisho.

71 [o]Wagershoni walipokea miji ifuatayo
pamoja na maeneo yake ya
malisho:
Katika nusu ya kabila la Manase:
walipewa Golani katika Bashani
na pia Ashtarothi.
72 [p]Kutoka kabila la Isakari
walipokea Kedeshi, Daberathi,
73 Ramothi na Anemu, pamoja na
maeneo yake ya malisho.
74 [q]Kutoka kabila la Asheri
walipokea Mashali, Abdoni,
75 [r]Hukoki na Rehobu, pamoja na
maeneo yake ya malisho.
76 Kutoka kabila la Naftali
walipokea Kedeshi katika Galilaya,

[a]**6:50** Kut 6:23; Hes 3; 2; 26:60; 1Nya 24:1; Ezr 7:2-5
[b]**6:53** 2Sam 8:17
[c]**6:54** Hes 31:10; 35:1-9; Yos 21:9-19
[d]**6:55** Yos 21:11-12
[e]**6:56** Yos 14:13; 15:13
[f]**6:57** Hes 33:20; Yos 15:48; 21:13
[g]**6:58** Yos 10:42
[h]**6:59** Yos 15:42; 21:16
[i]**6:60** Yer 1:1
[j]**6:63** Yos 21:7, 34
[k]**6:64** Hes 35:1-8; Yos 21:3, 41-42
[l]**6:67** Yos 10:33; Mwa 33:19; Yos 21:21
[m]**6:68** 1Fal 4:12; Yos 10:10
[n]**6:69** Yos 10:12; 19:45
[o]**6:71** 1Nya 23:7; Yos 20:8; 21:27
[p]**6:72** Yos 19:12
[q]**6:74** Yos 19:28
[r]**6:75** Yos 19:34; Hes 13:21

Hamoni na Kiriathaimu pamoja na maeneo yake ya malisho.

77 Wamerari (Walawi waliobakia) walipokea miji ifuatayo: kutoka kabila la Zabuloni walipokea Yokneamu, Karta, Rimoni na Tabori pamoja na maeneo yake ya malisho.
78 [a]Kutoka kabila la Reubeni, ng'ambo ya Yordani mashariki mwa Yeriko walipokea Bezeri ulioko jangwani, Yahasa,
79 [b]Kedemothi na Mefaathi pamoja na maeneo yake ya malisho.
80 [c]Na kutoka kabila la Gadi walipokea Ramothi huko Gileadi, Mahanaimu,
81 [d]Heshboni na Yazeri, pamoja na maeneo yake ya malisho.

*Wana Wa Isakari*

7 [e]Wana wa Isakari walikuwa: Tola, Pua, Yashubu na Shimroni; wote ni wanne.
2 [f]Wana wa Tola walikuwa: Uzi, Refaya, Yerieli, Yahmai, Ibsamu na Shemueli waliokuwa viongozi wa jamaa zao. Wakati wa utawala wa Mfalme Daudi, wazao wa Tola walioorodheshwa kama wapiganaji katika ukoo wao walikuwa watu 22,600.
3 [g]Mwana wa Uzi alikuwa: Izrahia.
Wana wa Izrahia walikuwa: Mikaeli, Obadia, Yoeli na Ishia. Wote hawa watano walikuwa wakuu wao.
4 Kulingana na ukoo wa jamaa zao, walikuwa na watu hodari wa vita wapatao 36,000, kwa sababu walikuwa na wanawake na watoto wengi.
5 Jamaa ya watu waliokuwa wapiganaji hodari kutoka koo zote za Isakari, kama ilivyoorodheshwa katika ukoo wao, jumla yao walikuwa 87,000.

*Wana Wa Benyamini*

6 [h]Wana watatu wa Benyamini walikuwa: Bela, Bekeri na Yediaeli.
7 Wana wa Bela walikuwa: Esboni, Uzi, Uzieli, Yeremothi na Iri; walikuwa viongozi wa jamaa zao; wote ni watano. Watu wapiganaji walioorodheshwa katika ukoo wao walikuwa 22,034.
8 Wana wa Bekeri walikuwa: Zemira, Yoashi, Eliezeri, Elioenai, Omri, Yeremothi, Abiya, Anathothi na Alemethi. Hawa wote walikuwa wana wa Bekeri.
9 [i]Orodha ya ukoo wao iliyoandikwa viongozi wa jamaa zao walikuwa wapiganaji 20,200.
10 Mwana wa Yediaeli alikuwa: Bilhani.
Wana wa Bilhani walikuwa: Yeushi, Benyamini, Ehudi, Kenaana, Zethani, Tarshishi na Ahishahari.
11 Hawa wana wote wa Yediaeli walikuwa viongozi wa jamaa zao. Kulikuwako wanaume wapiganaji 17,200 waliokuwa tayari kwenda vitani.
12 [j]Washupimu na Wahupimu walikuwa wazao wa Iri. Wahushimu walikuwa wazao wa Aheri.

*Wana Wa Naftali*

13 [k]Wana wa Naftali walikuwa: Yahzieli, Guni, Yeseri na Shalumu; hao walikuwa wazao wa Bilha.

[a]**6:78** Yos 20:8
[b]**6:79** Kum 2:26
[c]**6:80** Yos 20:8; Mwa 32:2
[d]**6:81** Hes 21:32; 2Nya 11:14; Kum 2:24; Yos 13:10; Isa 15:4; Yer 48:34
[e]**7:1** Mwa 30:18; Hes 26:23; Mwa 46:13
[f]**7:2** 2Sam 24:1-2; 1Nya 21:1-5; 27:1
[g]**7:3** 1Nya 5:24
[h]**7:6** Mwa 46:21; Hes 26:38
[i]**7:9** Kum 10:8
[j]**7:12** Hes 26:38-39
[k]**7:13** Mwa 30:8; 46:24

*Wana Wa Manase*

14 [a]Wana wa Manase walikuwa:

Asirieli alikuwa mzao wake
kutokana na suria wake wa Kiaramu.
Huyu suria akamzaa Makiri baba
wa Gileadi. 15 [b]Makiri akatwaa mke
kutoka miongoni mwa Wahupimu na
Washupimu. Jina la dada yake aliitwa
Maaka.

Mwana wa pili wa Makiri aliitwa
Selofehadi, ambaye alikuwa na
wasichana tu.

16 Maaka mkewe Makiri akamzaa
mwana aliyemwita Pereshi. Jina la
nduguye lilikuwa Shereshi. Wana wa
Pereshi walikuwa Ulamu na Rakemu.

17 [c]Mwana wa Ulamu alikuwa:
Bedani.
Hawa ndio waliokuwa wana wa
Gileadi mwana wa Makiri,
mwana wa Manase. 18 [d]Dada yake
aliyeitwa Hamolekethi aliwazaa
Ish-Hodi, Abiezeri na Mahla.
19 Wana wa Shemida walikuwa:
Ahiani, Shekemu, Liki na Aniamu.

*Wana Wa Efraimu*

20 [e]Wana wa Efraimu walikuwa:
Shuthela, ambaye alimzaa Beredi,
Beredi akamzaa Tahathi, Tahathi
akazaa Eleada,
Eleada akamzaa Tahathi,
21 Tahathi akamzaa Zabadi,
na Zabadi akamzaa Shuthela.

Ezeri na Eleadi waliuawa na wenyeji
wa Gathi walipokuwa wamekwenda
huko kuwanyang'anya mifugo yao.
22 [f]Baba yao Efraimu akawaombolezea
kwa siku nyingi, na jamaa zake wakaja
kumfariji. 23 [g]Kisha akakutana kimwili
na mke wake tena, naye akachukua
mimba, akamzalia mwana. Akamwita
Beria, kwa sababu ya misiba iliyoipata
nyumba yake. 24 [h]Beria alikuwa na
binti jina lake Sheera. Huyu ndiye
aliijenga miji ya Beth-Horoni ya Juu
na Beth-Horoni ya Chini, pamoja na
Uzen-Sheera.

25 Beria akamzaa pia Refa, naye Refa
akamzaa Reshefu,
Reshefu akamzaa Tela, Tela
akamzaa Tahani,
26 Tahani akamzaa Ladani, Ladani
akamzaa Amihudi,
Amihudi akamzaa Elishama,
27 [i]Elishama akamzaa Nuni,
Nuni akamzaa Yoshua.

28 [j]Nchi zao na makazi yao yalijumuisha
Betheli na vijiji vilivyouzunguka, Naarani
ilikuwa upande wa mashariki, Gezeri pamoja
na vijiji vyake upande wa magharibi, pia
Shekemu na vijiji vyake hadi kufikia Aya
na vijiji vyake. 29 [k]Katika mipaka ya Manase
walikuwepo Beth-Shani, Taanaki, Megido
na Dori pamoja na vijiji vyake. Wana wa
Yosefu mwana wa Israeli waliishi katika
miji hii.

*Wana Wa Asheri*

30 [l]Wana wa Asheri walikuwa:
Imna, Ishva, Ishvi na Beria. Dada
yao alikuwa Sera.
31 Wana wa Beria walikuwa:
Heberi na Malkieli, aliyekuwa
baba yake Birzaithi.
32 Heberi akawazaa Yafleti, Shomeri na
Hothamu, na Shua dada yao.
33 Wana wa Yafleti walikuwa:
Pasaki, Bimhali na Ashvathi.
Hawa walikuwa wana wa Yafleti.
34 Wana wa Shemeri walikuwa:

---

[a]**7:14** Mwa 41:51; Yos 17:1; Hes 26:30
[b]**7:15** Hes 26:33; 36:1-12; 27:1-11
[c]**7:17** Hes 26:30; 1Sam 12:11
[d]**7:18** Yos 17:2
[e]**7:20** Mwa 41:52; Hes 26:35; Mwa 48:14-20; Kum 33:13, 17; Za 60:7; 108:8
[f]**7:22** Mwa 37:34-35; Yos 7:6; 2Sam 3:31; Ay 2:11; Za 69:11; Yoe 2:13; Yn 1:19
[g]**7:23** Mwa 35:18; 1Sam 4:21; 1Nya 4:9
[h]**7:24** Yos 10:10; 16:3, 5; 16:3; 1Sam 13:18; 2Nya 8:5
[i]**7:27** Hes 13:8, 16
[j]**7:28** Yos 10:33; 16:7
[k]**7:29** Yos 17:11; 11:2; 1Fal 9:15; Amu 1:22-29
[l]**7:30** Mwa 40:17; Hes 26:44; Mwa 49:20; Kum 33:24

Ahi, Roga, Yehuba na Aramu.
35 Wana wa Helemu ndugu yake walikuwa:
Sofa, Imna, Sheleshi na Amali.
36 Wana wa Sofa walikuwa:
Sua, Harneferi, Shuali, Beri, Imra,
37 Bezeri, Hodu, Shama, Shilsha,
Ithrani[a] na Beera.
38 Wana wa Yetheri walikuwa:
Yefune, Pispa na Ara.
39 Wana wa Ula walikuwa:
Ara, Hanieli na Risia.

40 [b]Hawa wote ndio waliokuwa wazao wa Asheri, viongozi wa jamaa zao, watu bora, mashujaa walio hodari na viongozi maarufu. Idadi ya watu waliokuwa tayari kwa vita, kama ilivyoorodheshwa katika ukoo wao, walikuwa 26,000.

*Ukoo Wa Sauli Mbenyamini*

8 [c]Benyamini akamzaa: Bela mzaliwa wake wa kwanza,
Ashbeli mwanawe wa pili, Ahara mwanawe wa tatu,
2 Noha mwanawe wa nne na Rafa mwanawe wa tano.
3 [d]Wana wa Bela walikuwa:
Adari, Gera, Abihudi, 4 [e]Abishua, Naamani, Ahoa, 5 Gera, Shefufani na Huramu.
6 [f]Hawa ndio wazao wa Ehudi, waliokuwa viongozi wa jamaa za wale walioishi huko Geba na ambao walihamishiwa Manahathi:
7 Naamani, Ahiya na Gera. Gera alikuwa baba yao Uza na Ahihudi na ndiye aliwaongoza kwenda uhamishoni.
8 Shaharaimu aliwazaa wana katika nchi ya Moabu baada ya kuwapa talaka wake zake wawili yaani, Hushimu na Baara. 9 Kwa mkewe Hodeshi, akawazaa wana saba: Yobabu, Sibia, Mesha, Malkamu,
10 Yeuzi, Sakia na Mirma. Hawa ndio waliokuwa wanawe, viongozi wa jamaa zao. 11 Hushimu alimzalia: Abitubu na Elpaali.
12 [g]Wana wa Elpaali walikuwa:
Eberi, Mishamu, Shemedi (aliyeijenga miji ya Ono na Lodi, pamoja na vijiji vilivyoizunguka),
13 [h]na Beria na Shema, waliokuwa viongozi wa zile jamaa zilizokuwa zinaishi katika mji wa Aiyaloni, na ambao waliwafukuza wenyeji wa Gathi.
14 Wana wa Beria walikuwa Ahio, Shashaki, Yeremothi, 15 Zebadia, Aradi, Ederi, 16 Mikaeli, Ishpa, na Yoha.
17 Zebadia, Meshulamu, Hizki, Heberi,
18 Ishmerai, Izlia na Yobabu ndio waliokuwa wana wa Elpaali.
19 Yakimu, Zikri, Zabdi, 20 Elienai, Silethai, Elieli, 21 Adaya, Beraya na Shimrathi walikuwa wana wa Shimei.
22 Wana wa Shashaki walikuwa Ishpani, Eberi, Elieli, 23 Abdoni, Zikri, Hanani, 24 Hanania, Elamu, Anthothiya, 25 Ifdeya na Penueli.
26 Shamsherai, Sheharia, Athalia,
27 Yaareshia, Eliya na Zikri walikuwa wana wa Yerohamu.

28 Hawa wote walikuwa viongozi wa jamaa zao wakuu, kama ilivyoorodheshwa katika koo zao, nao waliishi Yerusalemu.

29 [i]Yeieli alikuwa baba yake Gibeoni naye aliishi huko Gibeoni.
Mke wake aliitwa Maaka.
30 Mwanawe mzaliwa wa kwanza alikuwa Abdoni, akafuatiwa na Suri, Kishi, Baali, Neri, Nadabu,
31 [j]Gedori, Ahio, Zekeri, 32 na Miklothi ambaye alikuwa baba yake Shimea. Hawa pia waliishi karibu na jamaa zao huko Yerusalemu.

---

[a]37 Kwa jina lingine Yetheri.
[b]**7:40** Kum 2:14
[c]**8:1** Mwa 46:21; 1Nya 7:6; Hes 26:38
[d]**8:3** Mwa 46:21
[e]**8:4** 2Sam 23:9
[f]**8:6** Amu 3:12-30; 1Nya 2:52; Neh 6:2
[g]**8:12** Ezr 2:33; Neh 7:37
[h]**8:13** Yos 10:12; Yn 11:22; Yos 19:42
[i]**8:29** Yos 9:3; 1Nya 9:35
[j]**8:31** 1Nya 9:37

33 [a]Neri akamzaa Kishi, Kishi akamzaa
Sauli, Sauli akamzaa Yonathani,
Malki-Shua, Abinadabu na
Esh-Baali.
34 [b]Yonathani akamzaa:
Merib-Baali,[c] naye Merib-Baali
akamzaa Mika.
35 Wana wa Mika walikuwa:
Pithoni, Meleki, Tarea na Ahazi.
36 Ahazi akamzaa Yehoada. Naye
Yehoada akawazaa Alemethi,
Azmawethi na Zimri, naye Zimri
akamzaa Mosa. 37 Mosa akamzaa
Binea, Binea akamzaa Rafa, na
mwanawe huyo ni Eleasa, na
mwanawe huyo ni Aseli.
38 Aseli alikuwa na wana sita; haya
ndiyo majina yao:
Azrikamu, Bokeru, Ishmaeli,
Shearia, Obadia na Hanani. Hawa
wote ndio waliokuwa wana wa
Aseli.
39 Wana wa Esheki, nduguye Aseli,
walikuwa:
Mzaliwa wake wa kwanza
alikuwa Ulamu, wa pili Yeushi
na wa tatu Elifeleti. 40 [d]Wana
wa Ulamu walikuwa mashujaa
hodari walioweza kutumia upinde.
Alikuwa na wana wengi na
wajukuu, jumla yao 150.
Hawa wote ndio walikuwa wazao wa
Benyamini.

9 [e]Waisraeli wote waliorodheshwa katika
koo zilizoandikwa kwenye kitabu cha
wafalme wa Israeli.

*Watu Katika Yerusalemu*

Watu wa Yuda walichukuliwa mateka
kwenda Babeli kwa sababu ya kukosa
uaminifu kwa Mungu. 2 [f]Basi watu wa
kwanza kurudi kukaa kwenye milki
zao katika miji yao walikuwa baadhi ya
Waisraeli, makuhani, Walawi na watumishi
wa Hekalu.[g]
3 [h]Wale waliotoka Yuda, Benyamini,
Efraimu na Manase ambao waliishi
Yerusalemu walikuwa:

*Jamaa Za Yuda*

4 [i]Uthai mwana wa Amihudi, mwana
wa Omri, mwana wa Imri, mwana
wa Bani, wa wana wa Peresi,
mwana wa Yuda.
5 Wazao wa Washiloni waliorudi ni:
Asaya mzaliwa wa kwanza na
wanawe.
6 Kwa wana wa Zera:
Yeueli.
Watu wa Yuda jumla yao
walikuwa watu 690.

*Jamaa Za Benyamini*

7 Kwa Benyamini walikuwa:
Salu mwana wa Meshulamu,
mwana wa Hodavia, mwana wa
Hasenua;
8 Ibneya mwana wa Yerohamu,
Ela mwana wa Uzi, mwana wa
Mikri; na Meshulamu mwana
wa Shefatia, mwana wa Reueli,
mwana wa Ibniya.
9 Watu kutoka Benyamini kama
walivyoorodheshwa katika koo
zao jumla yao ni 956. Watu hawa
wote walikuwa viongozi wa jamaa
zao.

*Jamaa Za Makuhani*

10 [j]Wa jamaa za makuhani walikuwa:
Yedaya, Yehoyaribu na Yakini;
11 Azaria mwana wa Hilkia, mwana
wa Meshulamu, mwana wa

---

[a] **8:33** 1Sam 28:19; 9:1; 14:49; 2Sam 2:8; Mdo 13:21
[b] **8:34** 2Sam 9:12; 4:4; 21:7-14
[c] 34 Merib-Baali maana yake ni Baali na Ashindane naye (Amu 6:32); ni jina lingine la mwana wa Yonathani, Mefiboshethi ambalo nalo maana yake ni Mtu wa Aibu (ona 2Sam 4:4).
[d] **8:40** Hes 26:38; 1Nya 12:2; 2Nya 11:1; 13:3; Neh 4:13; Wim 3:7-8; Efe 6:11-20
[e] **9:1** 1Nya 5:25
[f] **9:2** Yos 9:27; Ezr 2:70; 8:20; Neh 7:5; Law 26:33; 2Nya 33:11; 36:5
[g] 2 Yaani *Wanethini.*
[h] **9:3** Neh 11:1
[i] **9:4** Mwa 38:29; 46:12; Hes 26:20
[j] **9:10** Neh 11:10; 12:19

Sadoki, mwana wa Merayothi,
mwana wa Ahitubu aliyekuwa
afisa kiongozi wa nyumba ya
Mungu.
12 [a]Adaya mwana wa Yerohamu,
mwana wa Pashuri, mwana
wa Malkiya; Maasai, mwana
wa Adieli, mwana wa Yahzera,
mwana wa Meshulamu, mwana
wa Meshilemithi, mwana wa
Imeri.
13 Makuhani waliokuwa viongozi
wa jamaa zao walikuwa 1,760.
Walikuwa watu wenye uwezo,
waliowajibika kuhudumu katika
nyumba ya Mungu.

### *Jamaa Za Walawi*

14 [b]Jamaa za Walawi walikuwa:
Shemaya, mwana wa Hashubu,
mwana wa Azrikamu, mwana wa
Hashabia, wa wana wa Merari.
15 [c]Bakbakari, Hereshi, Galali na
Matania mwana wa Mika, mwana
wa Zikri, mwana wa Asafu.
16 [d]Obadia mwana wa Shemaya,
mwana wa Galali, mwana wa
Yeduthuni. Berekia mwana
wa Asa, mwana wa Elikana,
ambao waliishi katika vijiji vya
Wanetofathi.

### *Jamaa Za Mabawabu*

17 [e]Mabawabu katika Hekalu la Bwana
waliorudi walikuwa:
Shalumu, Akubu, Talmoni,
Ahimani na ndugu zao. Shalumu
alikuwa mlinzi wao mkuu.
18 [f]Walikuwa wamewekwa katika
lango la mfalme lililokuwa upande
wa mashariki, mpaka wakati
huu. Hawa walikuwa mabawabu
wa kutoka kwenye kambi ya
Walawi. 19 [g]Shalumu mwana wa
Kore, mwana wa Ebiasafu, mwana
wa Kora, pamoja na mabawabu
wenzake kutoka jamaa yake
ya Kora waliwajibika kulinda
malango ya Hema, kama vile baba
zao walivyokuwa wamewajibika
kulinda ingilio la Maskani ya
Bwana. 20 [h]Hapo zamani Finehasi
mwana wa Eleazari alikuwa
kiongozi wa mabawabu, naye
Bwana alikuwa pamoja naye:
21 [i]Zekaria mwana wa Meshelemia
alikuwa bawabu katika ingilio la
Hema la Kukutania.

22 [j]Jumla ya waliochaguliwa kuwa
mabawabu katika sakafu za kupuria nafaka
walikuwa watu 212. Waliandikishwa kwa
koo zao kwenye vijiji vyao. Mabawabu
hawa waliwekwa katika nafasi zao za
kuaminiwa na Daudi pamoja na mwonaji
Samweli. 23 Wao na wazao wao walikuwa
viongozi wa kulinda malango ya nyumba
ya Bwana, nyumba iliyoitwa Hema.
24 [k]Mabawabu walikuwa pande zote nne:
mashariki, magharibi, kaskazini na kusini.
25 [l]Ndugu zao katika vijiji vyao walikuwa
wakija mara kwa mara na kuwasaidia
katika kazi zao kwa vipindi mbalimbali
vya siku saba. 26 [m]Lakini mabawabu wanne
wakuu, waliokuwa Walawi, walikabidhiwa
wajibu kwa ajili ya vyumba na hazina
katika nyumba ya Mungu. 27 [n]Walikesha
mahali walipowekwa kuizunguka nyumba
ya Mungu, kwa sababu iliwapasa kuilinda.
Pia walitunza funguo kwa ajili ya kufungua
mlango kila siku asubuhi.
28 Baadhi yao walikuwa viongozi
wa kutunza vifaa vilivyotumika katika
huduma ndani ya Hekalu; walivihesabu kila
vilipoingizwa ndani na kila vilipotolewa.

[a]**9:12** Neh 10:3; Yer 38:1
[b]**9:14** 1Nya 6:19; Neh 11:15-19
[c]**9:15** 2Nya 20:14; Neh 11:22
[d]**9:16** Neh 12:28; 1Nya 2:54; Neh 7:26
[e]**9:17** Ezr 2:42; Neh 7:4; 1Nya 23:5; 26:1; Za 84:10
[f]**9:18** Eze 43:1; 46:1; 2Fal 11:19; Eze 44:23
[g]**9:19** Yer 35:4; Hes 26:9-11
[h]**9:20** Hes 25:7-13; Kut 6:25; Hes 3:32; 31:6; Yos 22:30-31; Za 106:30
[i]**9:21** 1Nya 26:2, 14
[j]**9:22** 1Nya 26:1; 2Nya 31:15, 18; 1Sam 9:9
[k]**9:24** 1Nya 26:13-19
[l]**9:25** 2Fal 11:5; 2Nya 23:8
[m]**9:26** 1Nya 26:22
[n]**9:27** Hes 3:38; 1Nya 23:30-32; 1Sam 22:22

29 [a]Wengine walipangiwa kutunza mapambo
na vifaa vingine vya patakatifu, pamoja na
unga, divai, mafuta, uvumba na vikolezo.
30 [b]Lakini baadhi ya makuhani walifanya
kazi ya kuchanganya vikolezo. 31 [c]Mlawi
aliyeitwa Matithia, mwana mzaliwa wa
kwanza wa Shalumu, wa ukoo wa Kora,
alikabidhiwa wajibu kwa ajili ya kuoka
mikate ya sadaka. 32 [d]Baadhi ya ndugu zao
wa ukoo wa Kohathi walikuwa viongozi wa
kuandaa mikate ya Wonyesho kwa ajili ya
kila Sabato, mikate iliyokuwa inawekwa
mezani.

33 [e]Wale waliokuwa waimbaji, viongozi
wa jamaa za Walawi, waliishi katika
vyumba vya Hekalu, nao hawakufanya
shughuli nyingine yoyote kwa sababu
iliwapasa kuwajibika kwa kazi hiyo usiku
na mchana.

34 Hawa wote walikuwa viongozi
wa jamaa za Walawi, wakuu kama
walivyoorodheshwa katika koo zao, nao
waliishi Yerusalemu.

*Ukoo Wa Sauli*

**(1 Nyakati 8:29-38)**

35 [f]Yeieli alikuwa baba yake Gibeoni
naye aliishi huko Gibeoni. Mke
wake aliitwa Maaka, 36 mwanawe
mzaliwa wa kwanza alikuwa
Abdoni, akafuatiwa na Suri, Kishi,
Baali, Neri, Nadabu, 37 Gedori,
Ahio, Zekaria na Miklothi.
38 Miklothi akamzaa Shimeamu.
Wao pia waliishi karibu na jamaa
zao huko Yerusalemu.

39 [g]Neri akamzaa Kishi, Kishi akamzaa
Sauli. Sauli akamzaa Yonathani,
Malki-Shua, Abinadabu na
Esh-Baali.[h]

40 [i]Yonathani akamzaa Merib-Baali,[j]
naye Merib-Baali akamzaa Mika.

41 [k]Wana wa Mika walikuwa:
Pithoni, Meleki, Tarea, na Ahazi.
42 Ahazi akamzaa Yara, Yara
akawazaa Alemethi, Azmawethi na
Zimri, naye Zimri akamzaa Mosa.
43 Mosa akamzaa Binea, Binea
akamzaa Refaya, na mwanawe
huyo ni Eleasa, na mwanawe huyo
ni Aseli.

44 Aseli alikuwa na wana sita, na haya
ndiyo majina yao:
Azrikamu, Bokeru, Ishmaeli,
Shearia, Obadia na Hanani. Hawa
ndio waliokuwa wana wa Aseli.

*Sauli Ajiua*

**(1 Samweli 31:1-13)**

10 [l]Basi Wafilisti wakapigana na Israeli.
Waisraeli wakawakimbia, na wengi
wakauawa katika mlima Gilboa. 2 Wafilisti
wakawafuatia kwa bidii Sauli na wanawe,
wakawaua Yonathani, Abinadabu na
Malki-Shua. 3 Mapigano yakawa makali
kumzunguka Sauli na wakati wapiga
mishale walipompata, wakamjeruhi.

4 [m]Sauli akamwambia mbeba silaha wake,
“Futa upanga wako unichome nao, la sivyo
hawa watu wasiotahiriwa watakuja na
kunidhalilisha.”

Lakini mbeba silaha wake akaogopa sana
wala hakuweza kufanya hivyo. Kwa hiyo
Sauli akachukua upanga wake mwenyewe
na kuuangukia. 5 Mbeba silaha wake
alipoona kwamba Sauli amekufa, naye pia
akauangukia upanga wake akafa. 6 Kwa
hiyo Sauli na wanawe watatu wakafa,
pamoja na nyumba yake yote.

7 Waisraeli wote waliokuwa bondeni
walipoona kwamba jeshi limekimbia na

[a]**9:29** Hes 3:23; 1Nya 23:29
[b]**9:30** Kut 30:25; 37:29; Yer 6:20; Eze 27:19-22; Mk 14:3
[c]**9:31** Law 24:5-8; 2Nya 13:11; Law 6:21
[d]**9:32** Kut 40:23; Ebr 9:2, 24; Yn 6:32, 33
[e]**9:33** 1Nya 25:1-31; 2Nya 5:12; Za 134:1; 1Nya 6:31; 13:8; 15:16
[f]**9:35** 1Nya 8:29
[g]**9:39** 1Nya 8:33; 1Sam 9:1; 13:22; 2Sam 2:8
[h]39 Anajulikana pia kwa jina la Ish-Boshethi, maana yake Mtu wa Aibu (2Sam 2:8).
[i]**9:40** 2Sam 4:4
[j]40 Pia anajulikana kwa jina la Mefiboshethi.
[k]**9:41** 2Sam 9:12; 1Nya 8:35
[l]**10:1** 1Sam 7:7; 13:5; 31:1
[m]**10:4** Amu 16:21

kwamba Sauli na wanawe wamekufa,
waliacha miji yao wakakimbia. Nao
Wafilisti wakaja na kukaa humo.
8 Kesho yake Wafilisti walipokuja
kuwavua maiti silaha, walimkuta Sauli
na wanawe wameanguka katika Mlima
Gilboa. 9 Wakamvua mavazi, wakachukua
kichwa chake pamoja na silaha zake,
wakawatuma wajumbe katika nchi yote ya
Wafilisti kutangaza habari hizi miongoni
mwa sanamu zao na watu wao. 10 [a]Waliweka
silaha zake katika hekalu la miungu yao,
wakatundika kichwa chake katika hekalu
la Dagoni.
11 [b]Wakazi wote wa Yabeshi-Gileadi
waliposikia yote Wafilisti waliyomtendea
Sauli, 12 mashujaa wao wote wakaondoka,
wakautwaa mwili wa Sauli na miili ya
wanawe, wakaileta Yabeshi. Wakaizika
mifupa yao chini ya mti mkubwa huko
Yabeshi, nao wakafunga kwa siku saba.
13 [c]Sauli alikufa kwa sababu hakuwa
mwaminifu kwa Bwana. Hakulishika
neno la Bwana, hata akataka shauri
kwa mwaguzi kwa ajili ya uongozi,
14 [d]hakumuuliza Bwana. Kwa hiyo Bwana
alimuua, na ufalme akampa Daudi mwana
wa Yese.

### *Daudi Atiwa Mafuta Kuwa Mfalme Wa Israeli*

**(2 Samweli 5:1-10)**

11 [e]Israeli yote walimjia Daudi kwa
pamoja huko Hebroni wakamwambia,
"Sisi ni nyama yako na damu yako.
2 [f]Zamani, wakati Sauli alikuwa mfalme,
wewe ndiwe uliyeiongoza Israeli vitani,
naye Bwana Mungu wako alikuambia,
'Wewe utawachunga watu wangu Israeli,
na utakuwa mtawala wao.' "
3 [g]Wazee wote wa Israeli walipokuwa
wamewasili kwa Mfalme Daudi huko
Hebroni, alifanya mapatano nao huko
Hebroni mbele za Bwana, nao wakamtia
Daudi mafuta awe mfalme wa Israeli,
sawasawa na Bwana alivyoahidi kupitia
kwa Samweli.

### *Daudi Ateka Yerusalemu*

4 [h]Daudi na Waisraeli wote wakaenda
Yerusalemu (ndio Yebusi). Nao Wayebusi
walioishi humo 5 wakamwambia Daudi,
"Wewe hutaingia humu." Hata hivyo, Daudi
akaiteka ngome ya Sayuni, Mji wa Daudi.
6 [i]Daudi alikuwa amesema, "Yeyote
aongozaye mashambulizi dhidi ya
Wayebusi, atakuwa jemadari mkuu."
Yoabu mwana wa Seruya akawa wa kwanza
kukwea, naye akawa mkuu.
7 [j]Daudi akafanya makao yake kwenye
ngome, hivyo ukaitwa Mji wa Daudi.
8 [k]Akajenga mji pande zote, kuanzia kwenye
mito hadi kwenye ukuta kuzunguka, wakati
huo huo Yoabu akajenga sehemu zingine
zilizobaki za Yerusalemu. 9 [l]Daudi akazidi
kuwa na nguvu zaidi na zaidi, kwa sababu
Bwana Mwenye Nguvu Zote alikuwa
pamoja naye.

### *Mashujaa Wa Daudi*

**(2 Samweli 23:8-39)**

10 [m]Hawa ndio waliokuwa wakuu wa
mashujaa wa Daudi: wao pamoja na
Israeli wote wakauimarisha ufalme wake
ili kuenea katika nchi yote, kama Bwana
alivyoahidi. 11 [n]Hii ndio orodha ya mashujaa
wa Daudi:
Yashobeamu, Mhakmoni, alikuwa mkuu
wa maafisa; yeye aliinua mkuki wake

---

[a]**10:10** Amu 16:23; 1Sam 31:10; Isa 48:5
[b]**10:11** Amu 21:8
[c]**10:13** 2Sam 1; 1; 15:23; 1Nya 5:25; 1Sam 13:13; Kum 18:9-14; 1Sam 28:7; 1Fal 18:18; 2Nya 16:9; Kut 22:18; Law 19:31; 20:27; 2Fal 21:6
[d]**10:14** 1Nya 12:23; 1Sam 13:14; 15:28
[e]**11:1** 1Nya 9:1; Mwa 13:18; 23:19; 2Sam 5:1; 1Nya 12:23
[f]**11:2** 1Sam 18:5, 16; Za 78:71; Mt 2:6; 1Nya 5:2
[g]**11:3** 1Sam 16:1-13; 2Sam 5:3; Rum 8:31
[h]**11:4** Yos 3:10; Amu 1:21; 2Sam 5:6; Mwa 10:16; 15:21; Kut 3:17; Amu 19:10
[i]**11:6** 2Sam 2:13; 8:16
[j]**11:7** 2Sam 5:7
[k]**11:8** 2Sam 5:9; 2Nya 32:5
[l]**11:9** 2Sam 3:1; Es 9:4
[m]**11:10** 1Nya 11:1; 12:23; 2Sam 23:8; 1Sam 16:1, 12
[n]**11:11** 2Sam 17:10

dhidi ya watu 300, ambao aliwaua katika
pambano moja.
12 Aliyefuata alikuwa Eleazari, mwana
wa Dodai, Mwahohi, mmojawapo wa
wale mashujaa watatu. 13 [a]Huyo alikuwa
pamoja na Daudi huko Pas-Damimu, wakati
Wafilisti walikusanyika huko kwa ajili ya
vita. Huko ambapo kulikuwa na shamba
lililokuwa limejaa shayiri, vikosi vya Israeli
vikawakimbia Wafilisti. 14 [b]Lakini Eleazari
na Daudi wakasimama imara katikati ya lile
shamba, nao wakalishindania na wakawaua
Wafilisti. Naye BWANA akawapa ushindi
mkubwa.
15 [c]Wakuu watatu miongoni mwa wale
thelathini, walimwendea Daudi katika
mwamba huko kwenye pango la Adulamu,
wakati kikundi cha Wafilisti kilikuwa
kimepiga kambi katika Bonde la Warefai.
16 [d]Wakati huo Daudi alikuwa katika
ngome, na kambi ya Wafilisti ilikuwa
huko Bethlehemu. 17 Daudi akatamani
maji, akasema, "Laiti mtu angenipatia
maji ya kunywa kutoka kisima kilichoko
karibu na lango la Bethlehemu!" 18 [e]Kwa
hivyo wale watatu, wakapita katikati ya
safu za Wafilisti, wakachota maji kutoka
kwa kisima kilicho karibu na lango la
Bethlehemu, wakamletea Daudi. Lakini
yeye akakataa kuyanywa. Badala yake,
aliyamimina mbele za BWANA. 19 Akasema,
"Mungu apishie mbali kwamba nifanye
hivi! Je kweli, niinywe damu ya watu hawa
waliohatarisha maisha yao?" Kwa sababu
walihatarisha maisha yao kuyaleta yale
maji, Daudi hakukubali kuyanywa.

Huo ndio uliokuwa ujasiri wa wale
mashujaa watatu.
20 [f]Abishai, ndugu yake Yoabu ndiye
alikuwa kiongozi wa hao Watatu. Aliinua
mkuki wake dhidi ya watu 300, ambao
aliwaua, kwa hiyo naye akawa na sifa
kama hao Watatu. 21 [g]Alitunukiwa heshima
maradufu ya wale Watatu, akawa jemadari
wao, ingawa hakuhesabiwa miongoni
mwao.
22 [h]Benaya, mwana wa Yehoyada alikuwa
mpiganaji hodari kutoka Kabseeli ambaye
alifanya mambo makubwa ya ujasiri.
Aliwaua mashujaa wawili waliokuwa
hodari kuliko wote wa Moabu. Pia alishuka
shimoni kulipokuwa na theluji na kumuua
simba. 23 [i]Alimuua Mmisri aliyekuwa na
urefu kama dhiraa tano.[j] Ingawa Mmisri
alikuwa na mkuki kama mti wa mfumaji
mkononi mwake, Benaya alimwendea na
rungu. Akamnyang'anya Mmisri mkuki
wake na kumuua nao. 24 Haya yalikuwa
mambo ya ushujaa ya Benaya mwana
wa Yehoyada; naye pia alikuwa maarufu
kama wale mashujaa watatu. 25 Yeye
aliheshimiwa zaidi ya wale Thelathini,
lakini hakujumuishwa miongoni mwa wale
Watatu: Daudi akamweka kuwa kiongozi
wa walinzi wake.

26 [k]Wale watu mashujaa walikuwa:
Asaheli nduguye Yoabu,
Elhanani mwana wa Dodo kutoka
Bethlehemu,
27 [l]Shamothi Mharori,
Helesi Mpeloni,
28 [m]Ira mwana wa Ikeshi kutoka
Tekoa,
Abiezeri kutoka Anathothi,
29 [n]Sibekai Mhushathi,
Ilai Mwahohi,
30 Maharai Mnetofathi,
Heledi mwana wa Baana,
Mnetofathi,
31 [o]Itai mwana wa Ribai kutoka Gibea
ya Benyamini,
Benaya Mpirathoni,
32 Hurai kutoka mabonde ya Gaashi,
Abieli Mwaribathi,

[a]**11:13** 1Sam 17:1
[b]**11:14** Kut 14:30; 1Sam 17:10; Mit 21:31
[c]**11:15** 1Nya 14:9
[d]**11:16** 2Sam 5:17
[e]**11:18** Kum 12:16
[f]**11:20** 1Sam 26:6
[g]**11:21** 2Sam 23:24; 1Nya 27:7
[h]**11:22** Yos 15:21; 1Sam 17:36; 2Sam 1:23; 23:20; 1Nya 12:8
[i]**11:23** 1Sam 26:6
[j]23 Dhiraa 5 ni sawa na mita 2.25.
[k]**11:26** 1Nya 2:18; 2Sam 23:24; 1Nya 27:7
[l]**11:27** 1Nya 27:8
[m]**11:28** 1Nya 27:12
[n]**11:29** 2Sam 21:18
[o]**11:31** 1Nya 27:14; Amu 12:13

33 Azmawethi Mbaharumi,
Eliaba Mshaalboni,
34 wana wa Hashemu Mgiloni,
Yonathani mwana wa Shagee
Mharari,
35 Ahiamu mwana wa Sakari
Mharari,
Elifale mwana wa Uru,
36 Heferi Mmekerathi,
Ahiya Mpeloni,
37 Hezro Mkarmeli,
Naarai mwana wa Ezbai,
38 Yoeli nduguye Nathani,
Mibhari mwana wa Hagri,
39 Seleki Mwamoni,
Naharai Mbeerothi, mbeba silaha
wa Yoabu mwana wa Seruya,
40 [a]Ira Mwithiri,
Garebu Mwithiri,
41 [b]Uria Mhiti,
Zabadi mwana wa Alai,
42 Adina mwana wa Shiza Mreubeni,
ambaye alikuwa mkuu wa
Wareubeni, akiwa pamoja na watu
thelathini,
43 Hanani mwana wa Maaka,
Yoshafati Mmithni,
44 [c]Uzia Mwashterathi,
Shama na Yeieli wana wa
Hothamu Mwaroeri,
45 Yediaeli mwana wa Shimri,
nduguye Yoha Mtizi,
46 Elieli Mmahawi,
Yeribai na Yoshavia wana wa
Elnaamu,
Ithma Mmoabu,
47 Elieli, na Obedi na Yaasieli
Mmesobai.

*Mashujaa Waungana Na Daudi*

12 [d]Hawa ndio watu waliomjia Daudi huko
Siklagi, wakati alikuwa amefukuzwa
mbele ya Sauli mwana wa Kishi (walikuwa
miongoni mwa mashujaa waliomsaidia
Daudi vitani, 2 [e]walikuwa na pinde na
walikuwa na uwezo wa kupiga mishale
au kutupa mawe kwa kombeo wakitumia
mkono wa kushoto au wa kulia; hawa
walikuwa ndugu zake Sauli kutoka kabila
la Benyamini):

3 [f]Mkuu wao alikuwa Ahiezeri, na wa
pili Yoashi, wote wana wa Shemaa
Mgibeathi; pia Yezieli na Peleti
wana wa Azmawethi; Beraka, Yehu
Mwanathothi, 4 [g]na Ishmaya Mgibeoni,
shujaa miongoni mwa wale Thelathini,
ambaye alikuwa kiongozi wa wale
Thelathini; Yeremia, Yahazieli,
Yohanani, Yozabadi, Mgederathi,
5 Eluzai, Yeremothi, Bealia, Shemaria,
Shefatia, Mharufi; 6 Elikana, Ishia,
Azareli, Yoezeri na Yashobeamu, wana
wa Kora; 7 [h]Yoela na Zebadia, wana wa
Yerohamu, kutoka Gedori.

8 [i]Baadhi ya Wagadi wakajitenga na
kujiunga na Daudi katika ngome yake huko
jangwani. Walikuwa mashujaa hodari,
waliokuwa tayari kwa vita na wenye uwezo
wa kutumia ngao na mkuki. Nyuso zao
zilikuwa nyuso za simba na walikuwa na
wepesi kama paa milimani.

9 Ezeri alikuwa mkuu wao,
Obadia alikuwa wa pili katika
uongozi, Eliabu wa tatu,
10 Mishmana wa nne, Yeremia wa tano,
11 Atai wa sita, Elieli wa saba,
12 Yohanani wa nane, Elzabadi wa tisa,
13 Yeremia wa kumi, na Makbanai wa
kumi na moja.

14 [j]Hawa Wagadi walikuwa majemadari.
Aliyekuwa wa mwisho kuliko wote aliweza
kuongoza askari 100, na aliyekuwa na
uweza zaidi ya wote aliongoza 1,000.
15 [k]Wao ndio walivuka Mto Yordani katika
mwezi wa kwanza ukiwa umefurika hadi
kwenye kingo zake zote na kusababisha

[a]**11:40** Yos 15:48; 1Nya 2:50-53
[b]**11:41** 2Sam 11:6; 1Nya 2:36
[c]**11:44** Kum 1:4
[d]**12:1** Yos 15:31; 1Sam 27:2-6
[e]**12:2** Amu 3:15; 20:16; 2Sam 3:19
[f]**12:3** Yos 21:18; 1Nya 11:28
[g]**12:4** Yos 15:36; 10:2; 18:21, 25; 1Fal 9:2; Isa 28:21
[h]**12:7** Yos 15:58
[i]**12:8** Mwa 30:11; 2Sam 2:18; 17:10; 23:14, 29; 23:20; 1Nya 2:17; Mit 28:1
[j]**12:14** Law 26:8; Kum 32:30
[k]**12:15** Yos 3:15; Yer 12:5; 49:19

watu wote waliokuwa wanaishi kwenye mabonde kukimbilia mashariki na wengine magharibi.
16 [a]Wabenyamini wengine na baadhi ya watu kutoka Yuda pia walikuja kwa Daudi
katika ngome yake. 17 [b]Daudi akatoka nje
kuwalaki na akawaambia, "Kama mmekuja kwangu kwa amani, kunisaidia, mimi niko tayari kuwaruhusu ninyi kuungana nami. Lakini kama mmekuja ili kunisaliti kwa adui zangu wakati mimi mikono yangu haina hatia, basi Mungu wa baba zetu aone na awahukumu."
18 [c]Kisha Roho akaja juu ya Amasai, mkuu wa wale Thelathini, naye akasema:

"Sisi tu watu wako, ee Daudi!
Nasi tuko pamoja na wewe, ee mwana wa Yese!
Ushindi, naam, ushindi uwe kwako,
pia ushindi kwa wale walio upande wako,
kwa kuwa Mungu wako atakusaidia."

Kwa hiyo Daudi akawapokea na kuwafanya viongozi wa vikosi vyake vya uvamizi.
19 [d]Baadhi ya watu kutoka kabila la Manase wakajiunga na Daudi wakati alikwenda pamoja na Wafilisti, kupigana na Sauli. (Daudi na watu wake hawakuwasaidia Wafilisti kwa sababu, baada ya ushauri, watawala wao walimrudisha. Wakasema, "Itatugharimu vichwa vyetu kama Daudi atatuasi na kurudi kwa Sauli bwana wake.")
20 [e]Daudi alipokwenda Siklagi, hawa ndio watu wa kabila la Manase waliojiunga naye: Adna, Yozabadi, Yediaeli, Mikaeli, Yozabadi, Elihu na Silethai, viongozi wa vikosi vya watu 1,000 katika kabila la
Manase. 21 Walimsaidia Daudi dhidi ya
makundi ya uvamizi, kwa kuwa wote walikuwa mashujaa hodari na walikuwa
majemadari katika jeshi lake. 22 Siku baada
ya siku watu walikuja kumsaidia Daudi, mpaka akawa na jeshi kubwa, kama jeshi la Mungu.

### *Wengine Waungana Na Daudi Huko Hebroni*

23 [f]Hawa ndio watu waliojiandaa kwa ajili ya vita waliokuja kwa Daudi huko Hebroni ili kumtwalia ufalme kutoka kwa Sauli, kama BWANA alivyokuwa amesema:

24 watu wa Yuda, wanaochukua ngao
na mikuki walikuwa 6,800 wote wakiwa tayari kwa vita.
25 Watu wa Simeoni, mashujaa
waliokuwa tayari kwa vita walikuwa 7,100.
26 Watu wa Lawi walikuwa 4,600,
27 pamoja na Yehoyada, kiongozi wa jamaa ya Aroni, aliyekuwa
pamoja na watu 3,700, 28 [g]na
Sadoki, kijana shujaa na hodari, aliyekuwa pamoja na maafisa ishirini na wawili kutoka jamaa yake.
29 [h]Watu wa Benyamini, ndugu zake
Sauli, walikuwa 3,000; wengi wao walikuwa wameendelea kuwa waaminifu kwa Sauli mpaka wakati huo.
30 Watu wa Efraimu, mashujaa hodari
20,800, watu waliokuwa maarufu katika koo zao.
31 Watu wa nusu ya kabila la Manase,
waliotajwa kwa majina ili waje kumweka Daudi kuwa mfalme, watu 18,000.
32 [i]Watu wa Isakari, waliofahamu
majira na kujua kile ambacho Israeli inapasa kufanya, walikuwa viongozi 200, pamoja na jamaa zao wote chini ya uongozi wao.
33 Watu wa Zabuloni, askari wenye
uzoefu mkubwa walioandaliwa tayari kwa vita wakiwa na silaha za kila aina, ili kumsaidia Daudi

[a]**12:16** 2Sam 3:19
[b]**12:17** Zek 3:2; Yud 9
[c]**12:18** Amu 6:34; 2Nya 15:1; 2Sam 17:25; 1Sam 25:5-6; 1Nya 2:17
[d]**12:19** 1Sam 29:2-4
[e]**12:20** 1Sam 27:6
[f]**12:23** 2Sam 2:3-4; 1Nya 10:14; 1Sam 16:1; 1Nya 11:10
[g]**12:28** 2Sam 8:17; 1Nya 27:17; 1Fal 1:8; 2:25; 1Nya 6:8; Eze 44:15
[h]**12:29** 2Sam 3:19; 2:8-9
[i]**12:32** Es 1:13

kwa uaminifu thabiti, walikuwa
50,000.
34 Watu wa Naftali, maafisa 1,000,
pamoja na watu 37,000
waliochukua ngao na mikuki.
35 Watu wa Dani 28,600 waliokuwa
tayari kwa vita.
36 Watu wa Asheri, askari 40,000
wenye uzoefu mkubwa
waliondaliwa kwa ajili ya vita.
37 Na pia watu kutoka mashariki ya
Yordani, watu wa Reubeni, Gadi
na nusu ya kabila la Manase,
wakiwa na kila aina ya silaha,
watu 120,000.

38 [a]Wote hawa walikuwa watu wapiganaji
waliojitolea kutumika katika safu zao.
Walikuja Hebroni wakiwa wameamua
kikamilifu kumfanya Daudi mfalme juu
ya Israeli yote. Waisraeli wengine wote
walikuwa pia na nia hiyo moja ya kumfanya
Daudi kuwa mfalme. 39 [b]Watu hawa
wakakaa huko na Daudi siku tatu, wakila
na kunywa, kwa sababu jamaa zao zilikuwa
zimewapatia mahitaji yao. 40 [c]Pia, majirani
zao hata wale walio mbali hadi Isakari,
Zabuloni na Naftali, walikuja wakiwaletea
vyakula walivyovibeba kwa punda, ngamia,
nyumbu na maksai. Kulikuwepo na wingi
wa unga, maandazi ya tini, maandazi ya
zabibu kavu, divai, mafuta, ng’ombe na
kondoo, kwa maana kulikuwa na furaha
katika Israeli.

*Kurudishwa Kwa Sanduku La Mungu*

**(2 Samweli 6:1-11)**

13 [d]Daudi alishauriana na kila afisa
wake, majemadari wa maelfu na
majemadari wa mamia. 2 [e]Ndipo Daudi
akaliambia kusanyiko lote la Israeli, “Kama
mkiona ni vyema, na kama ni mapenzi ya
Bwana Mungu wetu, tupeleke ujumbe
kwa ndugu zetu wengine walio mbali na
walio karibu katika nchi yote ya Israeli, pia
kwa makuhani na Walawi walio pamoja
nao katika miji yao na katika sehemu zao
za malisho yao, waje waungane na sisi.
3 [f]Sisi na tulirudishe Sanduku la Mungu
wetu kwetu kwa maana hatukujali wakati
wa utawala wa Sauli.” 4 Kusanyiko lote
likakubaliana kufanya hivyo, kwa sababu
ilionekana vyema kwa watu wote.
5 [g]Basi Daudi akawakusanya Waisraeli
wote, kuanzia Mto Shihori ulioko Misri
hadi Lebo-Hamathi, ili kulileta Sanduku
la Mungu kutoka Kiriath-Yearimu. 6 [h]Daudi
akiwa pamoja na Waisraeli wote wakaenda
Baala ya Yuda (yaani Kiriath-Yearimu)
kulipandisha Sanduku la Mungu Bwana,
yeye anayeketi katika kiti cha enzi kati ya
makerubi: Sanduku linaloitwa kwa Jina
lake, kutoka huko.
7 [i]Wakalisafirisha Sanduku la Mungu
kwa gari jipya la kukokotwa na maksai
kutoka nyumba ya Abinadabu, Uza na Ahio
wakiliongoza gari hilo. 8 [j]Daudi pamoja
na Waisraeli wote walikuwa wanasifu
kwa nguvu zao zote mbele za Mungu,
kwa nyimbo na kwa vinubi, zeze, matari,
matoazi na tarumbeta.
9 [k]Walipofika kwenye uwanja wa kupuria
nafaka wa Kidoni, Uza akaunyoosha mkono
wake ili kulizuia Sanduku, kwa sababu
maksai walijikwaa. 10 [l]Hasira ya Bwana
ikawaka dhidi ya Uza, akampiga kwa
sababu aliuweka mkono wake kwenye
Sanduku. Kwa hiyo akafa pale mbele za
Mungu.
11 [m]Ndipo Daudi akakasirika kwa sababu
ghadhabu ya Bwana ilifurika dhidi ya Uza,
mahali pale pakaitwa Peres-Uza[n] hadi leo.
12 Siku ile Daudi akamwogopa Mungu naye

[a]**12:38** 2Sam 5:1-3
[b]**12:39** 2Sam 3:20; Isa 25:6-8
[c]**12:40** 2Sam 16:1; 17:29; 1Sam 25:18; 1Nya 29:22
[d]**13:1** 1Nya 12:14; Za 132:1; Mit 15:22
[e]**13:2** 1Nya 10:7; Isa 37:4
[f]**13:3** 1Sam 7:1-2; 2Nya 1:5; 1Sam 23:2-4
[g]**13:5** 1Nya 11:1; 15:3; Yos 13:3; Hes 13:21; 1Sam 6:21; 7:2
[h]**13:6** Yos 15:9; 2Sam 6:2; Kut 25:22; 2Fal 19:15; 1Sam 4:4
[i]**13:7** Hes 4:15; 1Sam 7:1
[j]**13:8** 2Sam 6:5; Za 92:3
[k]**13:9** 2Sam 6:6
[l]**13:10** 1Nya 15:13, 15; Law 10:2; Hes 4:15
[m]**13:11** 1Nya 15:13; Za 7:11
[n]11 Maana yake ni Gadhabu dhidi ya Uza.

akauliza. “Nitawezaje kulichukua Sanduku
la Mungu kwangu?” 13 [a]Hakulichukua hilo
Sanduku akae nalo katika Mji wa Daudi.
Badala yake, akalipeleka nyumbani kwa
Obed-Edomu, Mgiti. 14 [b]Sanduku la Mungu
likabaki pamoja na jamaa ya Obed-Edomu,
nyumbani kwake kwa miezi mitatu, naye
BWANA akaibariki nyumba yake pamoja
na kila kitu alichokuwa nacho.

### *Nyumba Ya Daudi Na Jamaa Yake*

**(2 Samweli 5:11-16)**

14 [c]Basi Hiramu mfalme wa Tiro
akawatuma wajumbe kwa Daudi,
wakiwa na magogo ya mierezi, waashi na
maseremala ili kumjengea jumba la kifalme.
2 [d]Naye Daudi akatambua kwamba BWANA
amemwimarisha kuwa mfalme juu ya Israeli
na kwamba ufalme wake umetukuzwa kwa
ajili ya Israeli, watu wake.
3 [e]Huko Yerusalemu Daudi akaoa wake
wengine zaidi na akawa baba wa wana na
mabinti wengi. 4 [f]Haya ndiyo majina ya
watoto waliozaliwa kwake huko: Shamua,
Shobabu, Nathani, Solomoni, 5 Ibihari,
Elishua, Elpeleti, 6 Noga, Nefegi, Yafia,
7 Elishama, Beeliada na Elifeleti.

### *Daudi Awashinda Wafilisti*

**(2 Samweli 5:17-25)**

8 [g]Wafilisti waliposikia kuwa Daudi
ametiwa mafuta kuwa mfalme wa Israeli
yote, wakapanda na jeshi lao lote kwenda
kumsaka, lakini Daudi akapata habari hizo,
naye akatoka ili kwenda kukabiliana nao.
9 [h]Basi Wafilisti walikuwa wameingia na
kushambulia Bonde la Warefai, 10 Hivyo
Daudi akamuuliza Mungu: “Je, niende
kuwashambulia hao Wafilisti? Je, utawatia
mikononi mwangu?”
BWANA akamjibu, “Nenda, nitawatia
mikononi mwako.”
11 [i]Hivyo Daudi pamoja na watu
wake wakakwea mpaka Baal-Perasimu,[j]
akawashinda huko. Akasema, “Kama maji
yafurikavyo, Mungu amewafurikia adui
zangu kwa kutumia mkono wangu.” Kwa
hiyo mahali pale pakaitwa Baal-Perasimu.
12 [k]Wafilisti walikuwa wameacha miungu
yao huko, Daudi akaamuru iteketezwe kwa
moto.
13 [l]Kwa mara nyingine Wafilisti
wakavamia lile bonde; 14 [m]hivyo Daudi
akamuuliza Mungu tena, naye Mungu
akamjibu, “Usiwapandie moja kwa moja,
bali wazungukie na uwashambulie kutoka
mbele ya hiyo miti ya miforosadi. 15 Mara
usikiapo sauti ya kwenda juu ya hiyo miti
ya miforosadi, hapo ndipo utoke upigane
vita, kwa sababu hiyo itaonyesha kwamba
Mungu amekutangulia ili kupiga jeshi la
Wafilisti.” 16 [n]Kwa hiyo Daudi akafanya
kama alivyoagizwa na Mungu, wakalipiga
jeshi la Wafilisti kuanzia Gibeoni hadi
Gezeri.
17 [o]Hivyo umaarufu wa Daudi ukaenea
katika kila nchi, naye BWANA akayafanya
mataifa yote kumwogopa Daudi.

### *Sanduku La Agano Laletwa Yerusalemu*

**(2 Samweli 6:12-22)**

15 [p]Baada ya Daudi kujijengea nyumba
zake katika Mji wa Daudi, akatengeneza
sehemu kwa ajili ya Sanduku la Mungu,
kisha akasimamisha hema kwa ajili yake.
2 [q]Kisha Daudi akasema, “Hakuna mtu
yeyote anayeruhusiwa kulibeba Sanduku
la Mungu isipokuwa Walawi peke yao,

---

[a]**13:13** 1Nya 15:18, 24; 16:38; 26:4-5, 15
[b]**13:14** 2Sam 6:11; 1Nya 26:4-5; Mwa 30:27; 39:5; 1Nya 26:5; Za 37:22; Mit 3:9; 10:22; Mal 3:10
[c]**14:1** 1Fal 5:6; Hag 1:8; 2Sam 5:11
[d]**14:2** Hes 24:7; Kum 26:19
[e]**14:3** 1Nya 3:1; Kum 17:14-17
[f]**14:4** 2Sam 5:14; 1Nya 3:5
[g]**14:8** 1Nya 11:1; 2Sam 5:17; Za 2:1-5
[h]**14:9** Yos 15:8; 1Nya 11:15
[i]**14:11** Za 94:16; Isa 28:21
[j]11 Maana yake ni Bwana Afurikae.
[k]**14:12** Kut 32:20; Yos 7:15
[l]**14:13** 2Sam 5:22
[m]**14:14** Yos 8:6-7; 2Sam 5:23
[n]**14:16** Yos 9:3; 10:33; 2Sam 5:25
[o]**14:17** Yos 6:27; 2Nya 26:8; Kum 2:25; Za 2:1-12
[p]**15:1** Za 132:1-5; 2Sam 6:17; 1Nya 17:1-5; Mdo 7:46
[q]**15:2** Hes 3:6; Kum 31:9, 25; 2Nya 29:11; Hes 4:2, 15; Kum 10:5; Yos 3:3

kwa sababu BWANA aliwachagua kulibeba
Sanduku la BWANA na kuhudumu mbele
zake milele.”
3 [a]Daudi akawakusanya Israeli wote huko
Yerusalemu ili kulipandisha Sanduku la
BWANA na kulileta hadi kwenye sehemu
aliyokuwa ametengeneza kwa ajili yake.
4 Kisha Daudi akawakusanya pamoja wazao
wa Aroni na Walawi:

5 [b]Kutoka wazao wa Kohathi,
Urieli kiongozi na ndugu zake
120,
6 Kutoka wazao wa Merari,
Asaya kiongozi na ndugu zake
220.
7 Kutoka wazao wa Gershoni,[c]
Yoeli kiongozi na ndugu zake 130.
8 [d]Kutoka wazao wa Elisafani,
Shemaya kiongozi na ndugu zake
200.
9 [e]Kutoka wazao wa Hebroni,
Elieli kiongozi na ndugu zake 80.
10 Kutoka wazao wa Uzieli,
Aminadabu kiongozi na ndugu
zake 112.

11 [f]Kisha Daudi akawaita makuhani
Sadoki na Abiathari, pamoja na Walawi
Urieli, Asaya, Yoeli, Shemaya, Elieli na
Aminadabu. 12 [g]Akawaambia, “Ninyi ndio
viongozi wa jamaa za Walawi. Ninyi pamoja
na Walawi wenzenu inawapasa mjitakase na
kulipandisha Sanduku la BWANA, Mungu wa
Israeli hadi mahali ambapo nimetengeneza
kwa ajili yake. 13 [h]Ilikuwa ni kwa sababu hii,
ninyi Walawi, hamkulipandisha Sanduku la
BWANA mara ya kwanza, hata ikasababisha
BWANA Mungu wetu kuwaka hasira dhidi
yetu. Hatukumuuliza jinsi ya kufanya
ili tupate kulileta jinsi alivyoagiza.”
14 Kwa hiyo makuhani pamoja na Walawi
wakajitakasa ili kulipandisha Sanduku la
BWANA, Mungu wa Israeli. 15 [i]Nao Walawi
wakalichukua Sanduku la Mungu mabegani
mwao wakitumia mipiko, kama vile Mose
alivyoamuru sawasawa na neno la BWANA.
16 [j]Daudi akawaambia viongozi wa
Walawi kuwaweka ndugu zao waimbaji
ili waimbe nyimbo za shangwe, wakiwa
na vyombo vya uimbaji: zeze, vinubi na
matoazi.
17 [k]Basi Walawi wakawaweka Hemani
mwana wa Yoeli; kutoka miongoni mwa
ndugu zake, Asafu mwana wa Berekia;
kutoka miongoni mwa ndugu zao Wamerari,
Ethani mwana wa Kushaiya; 18 [l]hawa ndio
waliochaguliwa kuwa wasaidizi wao:
Zekaria, Yaazieli, Shemiramothi, Yehieli,
Uni, Eliabu, Benaya, Maaseya, Matithia,
Elifelehu, Mikneya, pamoja na mabawabu
Obed-Edomu na Yehieli.
19 [m]Waimbaji Hemani, Asafu na Ethani
walichaguliwa kupiga matoazi ya shaba;
20 Zekaria, Azieli, Shemiramothi, Yehieli,
Uni, Eliabu, Maaseya na Benaya walikuwa
wapiga zeze kufuatana na sauti ya *alamothi*,[n]
21 na Matithia, Elifelehu, Mikneya, Obed-
Edomu, Yehieli na Azazia walikuwa wapiga
vinubi, wakiongozwa kwa kufuata sauti ya
*sheminithi*.[o] 22 Kenania kiongozi wa Walawi
alikuwa msimamizi wa uimbaji; huu ndio
uliokuwa wajibu wake kwa sababu alikuwa
stadi katika hilo.
23 Berekia na Elikana walikuwa mabawabu
kwa ajili ya Sanduku. 24 [p]Shebania,
Yoshafati, Nethaneli, Amasai, Zekaria,
Benaya na Eliezeri, makuhani, walikuwa
wapiga tarumbeta mbele ya Sanduku la
Mungu. Obed-Edomu na Yehiya waliwekwa
pia kuwa mabawabu wa Sanduku.

---

[a] **15:3** 1Nya 13:5; 1Fal 8:1
[b] **15:5** Kut 6:16-18
[c] 7 Namna nyingine ya kutaja Gershomu.
[d] **15:8** Kut 6:22
[e] **15:9** Hes 26:58; Kut 6:18
[f] **15:11** 1Nya 12:28; 1Sam 22:20
[g] **15:12** Kut 29:10; Law 11:44; Eze 48:11; Yn 17:17; Law 10:3; 2Nya 5:11; 29:5, 15; Rum 12:1-2
[h] **15:13** 1Fal 8:4; 2Sam 6:3; 1Nya 13:11
[i] **15:15** Kut 25:14; Hes 4:5-15
[j] **15:16** Ezr 2:41; Neh 11:23; Amo 6:5; Ay 21:12; Za 68:25; 1Nya 6:31; 13:8; Za 33:2
[k] **15:17** 1Nya 6:33-44
[l] **15:18** 2Sam 6:10; 1Nya 26:4-5
[m] **15:19** 1Nya 16:12-13; 29:26
[n] 20 Huenda ni aina ya uimbaji.
[o] 21 Huenda ni aina ya uimbaji.
[p] **15:24** 2Nya 5:12; Hes 10:8; 2Nya 29:26; Za 81:3

25 [a]Basi Daudi pamoja na wazee wa Israeli
na majemadari wa vikosi vya elfu wakaenda
ili kulipandisha Sanduku la Agano la
BWANA kutoka nyumba ya Obed-Edomu
kwa shangwe. 26 [b]Kwa sababu Mungu
alikuwa amewasaidia Walawi waliokuwa
wanalichukua Sanduku la Agano la
BWANA, mafahali saba na kondoo dume
saba walitolewa dhabihu. 27 Basi Daudi
alikuwa amevaa joho la kitani safi, kama
walivyokuwa wamevaa Walawi wote
waliokuwa wanalichukua lile Sanduku,
waimbaji nao walivaa vivyo hivyo,
pamoja na Kenania aliyekuwa anaongoza
nyimbo za waimbaji. Daudi alivaa pia
kisibau cha kitani safi. 28 [c]Hivyo Israeli
wote wakalipandisha Sanduku la Agano
la BWANA kwa shangwe, wakipiga pembe
za kondoo dume, tarumbeta, matoazi,
wakipiga zeze na vinubi.

29 [d]Sanduku la Agano la BWANA
lilipokuwa linaingia katika Mji wa Daudi,
Mikali binti Sauli akachungulia dirishani.
Naye alipomwona Mfalme Daudi akicheza
na kusherehekea, akamdharau moyoni
mwake.

*Sanduku Lawekwa Ndani Ya Hema*

16 [e]Wakaleta Sanduku la Mungu na
kuliweka ndani ya hema ambalo Daudi
alikuwa amelisimamisha kwa ajili yake, na
wakatoa sadaka za kuteketezwa na sadaka
za amani mbele za Mungu. 2 [f]Baada ya Daudi
kumaliza kutoa hizo sadaka za kuteketezwa
na hizo sadaka za amani, akawabariki watu
katika jina la BWANA. 3 Kisha akamgawia
kila Mwisraeli mwanaume na mwanamke
mkate, andazi la tende na andazi la zabibu
kavu.

4 [g]Akawaweka pia baadhi ya Walawi ili
wahudumu mbele ya Sanduku la BWANA
kufanya maombi, kumshukuru na kumsifu
BWANA, Mungu wa Israeli: 5 Asafu ndiye
alikuwa mkuu wao, akisaidiwa na Zekaria,
Yeieli, Shemiramothi, Yehieli, Matithia,
Eliabu, Benaya, Obed-Edomu na Yeieli.
Hawa ndio wangepiga zeze na vinubi, Asafu
angepiga matoazi, 6 nao Benaya na Yahazieli
makuhani, ndio wangepiga tarumbeta mara
kwa mara mbele ya Sanduku la Agano la
Mungu.

*Zaburi Ya Daudi Ya Shukrani*

**(Zaburi 105:1-15; 96:1-13; 106:1, 47-48)**

7 [h]Siku ile, kitu cha kwanza Daudi
alichofanya ni kumkabidhi Asafu na
wenzake zaburi hii ya shukrani kwa
BWANA:

8 [i]Mshukuruni BWANA, liitieni jina
lake;
wajulisheni mataifa yale
aliyoyatenda.
9 [j]Mwimbieni yeye, mwimbieni yeye
sifa;
waambieni matendo yake yote ya
ajabu.
10 [k]Lishangilieni jina lake takatifu;
mioyo ya wale wamtafutao
BWANA na ifurahi.
11 [l]Mtafuteni BWANA na nguvu zake;
utafuteni uso wake siku zote.
12 [m]Kumbuka matendo ya ajabu
aliyoyafanya,
miujiza yake na hukumu
alizozitamka,
13 enyi wazao wa Israeli mtumishi
wake,
enyi wana wa Yakobo, wateule
wake.

14 [n]Yeye ndiye BWANA Mungu wetu;
hukumu zake zimo duniani pote.

[a]**15:25** 2Sam 16:12-13; 2Nya 5:2; Yer 3:16; Kum 12:7, 18; Ezr 6:16
[b]**15:26** Ay 42:8; Hes 23:1-4, 29
[c]**15:28** Kut 19:13; 1Nya 13:8
[d]**15:29** 2Sam 6:16; Mdo 2:13
[e]**16:1** 2Sam 6:17-19
[f]**16:2** Kut 39:43; Hes 6:23-27
[g]**16:4** 1Nya 15:1-2
[h]**16:7** 2Sam 23:1; Za 47:7
[i]**16:8** Za 107:1; 118:1; 2Fal 19:19
[j]**16:9** Za 100:1; Kut 15:1; Za 7:17; 95:1-2
[k]**16:10** Za 34:3; Isa 45:25
[l]**16:11** Za 27:8; Mit 8:17; Amo 5:6-14
[m]**16:12** Za 78:43; 103:2
[n]**16:14** Isa 29:9; 4:4

15 Hulikumbuka agano lake milele,
neno ambalo aliamuru, kwa vizazi elfu,
16 [a]agano alilolifanya na Abrahamu,
kiapo alichomwapia Isaki.
17 [b]Alilithibitisha kwa Yakobo kuwa amri,
kwa Israeli liwe agano la milele:
18 [c]"Nitakupa wewe nchi ya Kanaani
kuwa sehemu utakayoirithi."

19 [d]Walipokuwa wachache kwa idadi,
wachache sana na wageni ndani yake,
20 walitangatanga kutoka taifa moja hadi jingine,
kutoka ufalme mmoja hadi mwingine.
21 [e]Hakuruhusu mtu yeyote awaonee;
kwa ajili yao aliwakemea wafalme, akisema:
22 [f]"Msiwaguse niliowatia mafuta;
msiwadhuru manabii wangu."

23 [g]Mwimbieni BWANA dunia yote;
tangazeni wokovu wake siku baada ya siku.
24 [h]Tangazeni utukufu wake katikati ya mataifa,
matendo yake ya ajabu miongoni mwa mataifa yote.
25 [i]Kwa kuwa BWANA ni mkuu,
mwenye kustahili kusifiwa kuliko wote;
yeye ni wa kuogopwa kuliko miungu yote.
26 [j]Kwa maana miungu yote ya mataifa ni sanamu,
lakini BWANA aliziumba mbingu.
27 Fahari na enzi viko mbele yake;
nguvu na utukufu vimo patakatifu pake.
28 [k]Mpeni BWANA, enyi jamaa za mataifa,
mpeni BWANA utukufu na nguvu,
29 mpeni BWANA utukufu
unaostahili jina lake.
Leteni sadaka na mje katika nyua zake;
mwabuduni BWANA katika uzuri wa utakatifu wake.
30 [l]Dunia yote na itetemeke mbele zake!
Ulimwengu ameuweka imara;
hauwezi kusogezwa.
31 [m]Mbingu na zishangilie, nchi na ifurahi;
semeni katikati ya mataifa,
"BWANA anatawala!"
32 [n]Bahari na ivume, na vyote vilivyomo ndani yake;
mashamba na yashangilie, na vyote vilivyomo ndani yake.
33 [o]Kisha miti ya msituni itaimba,
itaimba kwa furaha mbele za BWANA,
kwa maana anakuja kuihukumu dunia.

34 [p]Mshukuruni BWANA kwa kuwa ni mwema;
upendo wake wadumu milele.
35 [q]Mlilieni, "Ee Mungu Mwokozi wetu, tuokoe.
Tukusanye tena na utukomboe
kutoka kwa mataifa,

[a]**16:16** Mwa 17:2; Neh 9:8; Ebr 6:13-18; Za 105:8-10; Mwa 15:18; 26:3
[b]**16:17** Mwa 35:9-12
[c]**16:18** Mwa 13:14-17
[d]**16:19** Mwa 34:30; Ebr 11:13; Kum 7:7
[e]**16:21** Mwa 20:3; Kut 7:15-18; Za 9:5; Mwa 12:17
[f]**16:22** Mwa 20:7; Za 105; 15; 1Yn 2:27
[g]**16:23** Za 47:1; 96:1
[h]**16:24** Isa 12:4
[i]**16:25** Za 18:3; 76:7; 89:7; Kut 18:11; Isa 40:25-26; Za 24:8
[j]**16:26** Law 19:4; Isa 45:20; 1Kor 8:4; Za 115:4-8; Yer 10:3
[k]**16:28** Za 29:1-2; 8:1
[l]**16:30** Za 2:11; 33:8
[m]**16:31** Isa 44:23; 35:10; 49:13; Mao 5:19; Isa 52:7; Lk 2:13; Ufu 14:2
[n]**16:32** Kut 20:11; Za 98:7; 96:10
[o]**16:33** Isa 14:8; 55:12; Za 110:6
[p]**16:34** Isa 12:4; Za 25:7; Ezr 3:11; Yer 33:1
[q]**16:35** Kum 32:15; Mik 7:7; Ezr 3:11; Yer 33:11; Za 106:47

ili tuweze kulishukuru jina lako
takatifu,
na kushangilia katika sifa zako."
36 [a]Atukuzwe Bwana, Mungu wa
Israeli,
tangu milele na hata milele.

Nao watu wote wakasema, "Amen," na "Msifuni Bwana."

37 Daudi akamwacha Asafu na wenzake
mbele ya Sanduku la Agano la Bwana ili
wahudumu humo mara kwa mara, kulingana
na mahitaji ya kila siku. 38 [b]Pia akamwacha
Obed-Edomu pamoja na wenzake sitini na
wanane wahudumu pamoja nao. Obed-Edomu mwana wa Yeduthuni na pia Hosa
walikuwa mabawabu wa lango.
39 [c]Daudi akamwacha kuhani Sadoki
pamoja na makuhani wenzake mbele ya
hema ya ibada ya Bwana katika mahali pa
juu pa kuabudia huko Gibeoni 40 [d]ili kutoa
sadaka za kuteketezwa kwa Bwana kwenye
madhabahu ya sadaka ya kuteketezwa mara
kwa mara, asubuhi na jioni, sawasawa na
kila kitu kilichoandikwa katika sheria
ya Bwana ambayo alikuwa amempa
Israeli. 41 [e]Waliohudumu pamoja nao
walikuwa Hemani, Yeduthuni na wale wote
waliochaguliwa na kutajwa kwa jina kumpa
Bwana shukrani, "Kwa maana fadhili zake
zadumu milele." 42 [f]Hemani na Yeduthuni
walikuwa na wajibu wa kupiga tarumbeta,
matoazi na kutumia vyombo vingine kwa
ajili ya nyimbo za sifa kwa Mungu. Wana
wa Yeduthuni waliwekwa langoni.
43 [g]Kisha watu wote wakaondoka, kila
mmoja akarudi nyumbani kwake, naye
Daudi akarudi nyumbani kuibariki jamaa
yake.

[a]**16:36** Kum 27:15; 1Fal 8:15; Neh 8:6; 10:27; 2Nya 8:14; Za 72:18-19
[b]**16:38** 1Nya 13:13; 26:4-10
[c]**16:39** 1Sam 2:35; 1Nya 21:29; 2Sam 8:17; Yos 9:3; 1Fal 3:4
[d]**16:40** Kut 29:38; Hes 28:1-8
[e]**16:41** 1Nya 15:19; 2Nya 5:13; Yak 5:11; Ezr 3:11; Neh 9:17; Za 25:10; 33:5; Yer 33:11; Yoe 2:13; Lk 3:36
[f]**16:42** 2Nya 7:6
[g]**16:43** 2Sam 6:19-20; Mwa 18:19; Yos 24:15

*Ahadi Ya Mungu Kwa Daudi*

**(2 Samweli 7:1-17)**

17 [h]Baada ya Daudi kuingia rasmi katika
jumba lake la kifalme, akamwambia
nabii Nathani, "Hebu tazama, mimi ninakaa
kwenye nyumba nzuri iliyojengwa kwa
mierezi, wakati Sanduku la Agano la
Bwana liko ndani ya hema."
2 [i]Nathani akamjibu Daudi, "Lolote ulilo
nalo moyoni mwako litende, kwa maana
Mungu yu pamoja nawe." 3 Usiku ule neno
la Mungu likamjia Nathani, kusema:

4 [j]"Nenda ukamwambie mtumishi
wangu Daudi, 'Hili ndilo asemalo
Bwana: Wewe hutanijengea mimi
nyumba ili nikae humo. 5 [k]Mimi
sijakaa ndani ya nyumba tangu siku ile
niliyowatoa Israeli kutoka Misri mpaka
leo. Nimehama kutoka hema moja hadi
jingine na kutoka mahali pamoja hadi
pengine. 6 Je, popote nilipokwenda
pamoja na Waisraeli wote, wakati
wowote nilimwambia kiongozi yeyote
niliyemwagiza kuwachunga watu
wangu, kwa nini hujanijengea nyumba
ya mierezi?'
7 [l]"Sasa basi, mwambie mtumishi
wangu Daudi, 'Hili ndilo asemalo
Bwana Mwenye Nguvu Zote:
Nilikuchukua machungani na kutoka
kuandama kondoo ili uwatawale watu
wangu Israeli. 8 Nimekuwa pamoja
nawe popote ulipokwenda, nami
nimekuondolea mbali adui zako wote
mbele yako. Basi nitalifanya jina
lako kuwa kuu kama majina ya watu
walio wakuu sana duniani. 9 [m]Nami
nitawapatia watu wangu Israeli mahali
na nitawapa ili wawe na mahali pao
wenyewe pa kuishi na wasisumbuliwe
tena. Watu waovu hawatawaonea tena,
kama walivyofanya mwanzoni, 10 [n]na

[h]**17:1** Mdo 7:46; 1Nya 15:1
[i]**17:2** 1Nya 22:7; 2Nya 6:7
[j]**17:4** 1Nya 28:3
[k]**17:5** 2Sam 6:21; Kut 40:2; 1Fal 8:4, 16
[l]**17:7** 2Sam 6:21
[m]**17:9** 2Nya 15:2; Isa 49:17; Yer 31:12; Eze 34:14
[n]**17:10** Amu 2:16

ambavyo wamefanya siku zote tangu
nilipowachagua viongozi kwa ajili ya
watu wangu Israeli. Pia nitawatiisha
adui zenu wote.
"'Pamoja na hayo ninakuambia
kwamba BWANA atakujengea
nyumba: 11 Wakati wako utakapokuwa
umekwisha, nawe ukawa umekwenda
kukaa na baba zako, nitamwinua mzao
wako aingie mahali pako kuwa mfalme,
mmoja wa wana wako mwenyewe, nami
nitaufanya imara ufalme wake. 12 [a]Yeye
ndiye atakayejenga nyumba kwa ajili
yangu, nami nitakifanya imara kiti cha
ufalme wake milele. 13 [b]Mimi nitakuwa
baba yake, naye atakuwa mwanangu.
Kamwe sitaondoa upendo wangu
kwake, kama nilivyouondoa kwa yeye
aliyekutangulia. 14 [c]Nitamweka juu
ya nyumba yangu na ufalme wangu
milele; kiti chake cha enzi nitakifanya
imara milele.'"

15 Nathani akamwarifu Daudi maneno
yote ya maono haya.

*Maombi Ya Daudi*

**(2 Samweli 7:18-29)**

16 [d]Ndipo Mfalme Daudi akaingia ndani,
akaketi mbele za BWANA, akasema:

"Mimi ni nani, Ee BWANA Mungu,
na jamaa yangu ni nini, hata umenileta
mpaka hapa nilipo? 17 Kana kwamba
hili halitoshi machoni pako, Ee
Mungu, umenena pia kuhusu siku
zijazo za nyumba ya mtumishi wako.
Umeniangalia kama mtu aliyetukuka
kuliko watu wote, Ee BWANA Mungu.
18 [e]"Daudi aweza kukuambia nini
zaidi kuhusu kumheshimu mtumishi
wako? Kwa maana wewe unamjua
mtumishi wako, 19 [f]Ee BWANA Mungu.
Kwa ajili ya mtumishi wako, tena
sawasawa na mapenzi yako, umefanya
jambo hili kubwa sana na kujulisha
ahadi hizi zote zilizo kubwa sana.
20 [g]"Hakuna aliye kama wewe, Ee
BWANA Mungu, wala hakuna Mungu
ila wewe, kama vile tulivyosikia kwa
masikio yetu wenyewe. 21 [h]Naye ni nani
aliye kama watu wako Israeli: taifa
pekee duniani ambalo Mungu wake
alitoka kwenda kulikomboa kwa ajili
yake mwenyewe na kujifanyia jina kwa
ajili yake mwenyewe, kwa kufanya
maajabu makubwa na ya kutisha kwa
kuwafukuza mataifa mbele ya watu
wako, ambao uliwakomboa kutoka
Misri? 22 [i]Uliwafanya watu wako Israeli
kuwa watu wako wewe mwenyewe
milele, nawe, Ee BWANA Mungu,
umekuwa Mungu wao.
23 [j]"Sasa basi, BWANA ahadi
uliyoweka kuhusu mtumishi wako
na nyumba yake na uithibitishe
milele. Fanya kama ulivyoahidi, 24 [k]ili
ithibitike na jina lako litakuwa kuu
milele. Kisha watu watasema, 'BWANA
Mungu Mwenye Nguvu Zote, Mungu
aliye juu ya Israeli, ndiye Mungu wa
Israeli.' Nayo nyumba ya mtumishi
wako Daudi itafanywa imara mbele
zako.
25 "Wewe, Mungu wangu,
umemfunulia mtumishi wako Daudi
kwamba utamjengea yeye nyumba.
Hivyo mtumishi wako amekuwa na
ujasiri wa kukuomba maombi haya.
26 [l]Ee BWANA, wewe ndiwe Mungu!
Umemwahidi mtumishi wako mambo

---

[a]**17:12** 1Fal 5:5; 2Nya 7:18; 13:5
[b]**17:13** 2Kor 6:18; 2Sam 7:14-15; Ebr 1:5; Lk 1:32; 1Nya 28:6; 22:10
[c]**17:14** 1Fal 2:12; 2Nya 9:8; Za 132:11; Yer 33:17; Za 2:6; 89:36; Isa 9:7; Eze 37:25; Dan 2:44; 7:14-27; Mt 21:1-11; Lk 1:33; Ebr 1:8
[d]**17:16** 2Sam 7:18; 2Fal 19:14; Ay 7:14-17; Mwa 32:10; Za 144:3
[e]**17:18** Za 139:1; Yn 21:17
[f]**17:19** 2Sam 7:16-17, 25; 2Fal 20:6; Mt 11:26; Efe 1:11
[g]**17:20** Kut 8:10; Kum 3:24; Isa 44:6; Kut 15:11; Kum 33:26; 1Sam 2:2; 2Sam 7:22; Za 86:8
[h]**17:21** Kut 6:6
[i]**17:22** Kut 19:5-6
[j]**17:23** 1Fal 8:25
[k]**17:24** 2Nya 6:33; Yn 12:28; Za 21:13; 72:19; Mt 6:9, 13
[l]**17:26** Kut 34:6; Ebr 6:18

haya mazuri. 27 [a]Basi imekupendeza
kuibariki nyumba ya mtumishi wako,
ili idumu milele machoni pako; kwa
ajili yako, Ee BWANA, umeibariki, nayo
itabarikiwa milele."

*Ushindi Wa Daudi*

**(2 Samweli 8:1-18)**

18 Baada ya muda, Daudi akawashinda
Wafilisti na kuwatiisha, naye akautwaa
Gathi pamoja na vijiji vinavyouzunguka
kutoka utawala wa Wafilisti.
2 [b]Pia Daudi akawashinda Wamoabu,
wakawa watumishi wake, nao wakawa
wanamletea ushuru.
3 [c]Zaidi ya hayo, Daudi akapigana na
Hadadezeri mfalme wa Soba, hadi Hamathi,
wakati alikwenda kuimarisha utawala wake
katika Mto Frati. 4 [d]Daudi akateka magari
ya vita 1,000 miongoni mwa magari yake,
waendesha hayo magari ya kukokotwa na
farasi 7,000 na askari wa miguu 20,000.
Daudi akakata mishipa ya miguu ya nyuma
ya farasi wote wakokotao magari, ila
akabakiza 100.
5 [e]Waaramu wa Dameski, walipokuja
kumsaidia Hadadezeri mfalme wa Soba,
Daudi akawashambulia na kuwaua 22,000
miongoni mwao. 6 [f]Daudi akaweka askari
walinzi katika ufalme wa Waaramu huko
Dameski. Basi Waaramu wakawa watumwa
wa Daudi, na kumlipa ushuru. BWANA
akampa Daudi ushindi kote alipokwenda.
7 Daudi akazitwaa ngao za dhahabu
zilizokuwa za maafisa wa Hadadezeri
na kuzileta Yerusalemu. 8 [g]Kutoka miji
ya Tibhathi na Kuni, iliyokuwa miji
ya Hadadezeri, Daudi akatwaa shaba
nyingi sana, ambayo Solomoni aliitumia
kutengenezea ile Bahari ya shaba, zile
nguzo na vifaa mbalimbali vya shaba.
9 Tou mfalme wa Hamathi aliposikia
kwamba Daudi amelishinda jeshi lote la
Hadadezeri mfalme wa Soba, 10 [h]akamtuma
mwanawe, Hadoramu kwa Mfalme Daudi
ili kumsalimu na kumpongeza kwa
ushindi wake katika vita dhidi ya Mfalme
Hadadezeri, kwa kuwa alikuwa amepigana
vita mara nyingi na Tou. Hadoramu
akamletea Daudi vifaa mbalimbali vya
dhahabu, fedha na shaba.
11 [i]Mfalme Daudi akaviweka vifaa hivi
wakfu kwa BWANA kama vile alivyokuwa
amefanya kwa fedha na dhahabu aliyokuwa
ameitwaa katika mataifa yote haya:
Edomu na Moabu, Waamoni, Wafilisti na
Waamaleki.
12 [j]Abishai mwana wa Seruya akawaua
Waedomu 18,000 katika Bonde la Chumvi.
13 [k]Akaweka kambi za askari walinzi huko
Edomu, nao Waedomu wote wakawa
watumishi wa Daudi. BWANA akampa
Daudi ushindi kila alipokwenda.

*Maafisa Wa Daudi*

14 [l]Daudi akatawala Israeli yote, akitenda
lililo haki na sawa kwa watu wake wote.
15 [m]Yoabu mwana wa Seruya alikuwa
jemadari wa jeshi; Yehoshafati mwana wa
Ahiludi alikuwa mweka kumbukumbu;
16 [n]Sadoki mwana wa Ahitubu na Ahimeleki
mwana wa Abiathari walikuwa makuhani;
Shausha alikuwa mwandishi; 17 [o]naye
Benaya mwana wa Yehoyada alikuwa
msimamizi wa Wakerethi na Wapelethi; nao
wana wa Daudi walikuwa maafisa wakuu
katika utumishi wa mfalme.

---

[a]**17:27** Za 16:11; 21:6; Rum 11:29; Mwa 27:33; Za 72:17
[b]**18:2** Hes 24:17; 21:29
[c]**18:3** 1Nya 19:6; Mwa 2:14; 15:18; Kum 11:24; 2Sam 8:3
[d]**18:4** Mwa 49:6; 2Sam 8:4
[e]**18:5** 2Fal 16:9; 1Nya 19:6
[f]**18:6** 1Nya 17:8; Mit 21:31; Za 91:14; 121:8
[g]**18:8** 1Fal 7:23; 2Nya 4:12-16
[h]**18:10** 2Sam 8:10
[i]**18:11** Hes 24:18-20
[j]**18:12** 1Fal 11:15; 2Sam 7:13; 2Fal 14:7; 2Nya 25:11
[k]**18:13** Mwa 27:29; Hes 24:18; 1Sam 10:3; 13:3; 14:1
[l]**18:14** 1Nya 29:26; 11:1-6
[m]**18:15** 2Sam 5:6-8
[n]**18:16** 2Sam 8:17; 1Nya 6:8; 24; 6
[o]**18:17** 1Sam 30:14; 2Sam 8:18

*Vita Dhidi Ya Waamoni*

**(2 Samweli 10:1-19)**

19 [a]Baada ya muda, Nahashi mfalme
wa Waamoni akafa, mwanawe
akaingia mahali pake. 2 Daudi akawaza,
“Nitamtendea wema Hanuni mwana wa
Nahashi, kwa sababu baba yake alinitendea
wema.”

Hivyo Daudi akatuma wajumbe ili
kumfariji Hanuni kwa ajili ya kifo cha
baba yake. Watu wa Daudi walipofika
kwa Hanuni katika nchi ya Waamoni
ili kumfariji, 3 [b]wakuu wa Waamoni
wakamwambia Hanuni, “Hivi unadhani
Daudi anamheshimu baba yako kwa
kuwatuma wajumbe kukufariji? Je, hawa
watu hawakuja kuipeleleza na kuidadisi
nchi ili waishinde?” 4 Kwa hiyo Hanuni
akawakamata watu wa Daudi, akawanyoa
ndevu akakata nguo zao katikati kwenye
matako, akawaacha waende zao.

5 [c]Mtu mmoja alipofika na kumpasha
Daudi habari za watu hawa, akawatuma
wajumbe wengine kuwalaki, kwa maana
walikuwa wamevunjiwa heshima sana.
Mfalme akasema, “Kaeni huko Yeriko
mpaka ndevu zenu ziote, ndipo mje.”

6 [d]Waamoni walipotambua kuwa
wamekuwa machukizo kwa Daudi, Hanuni
na Waamoni wakatuma talanta 1,000[e]
za fedha ili kukodisha magari ya vita
pamoja na waendeshaji wa hayo magari
ya kukokotwa na farasi, kutoka Aramu-
Naharaimu,[f] Aramu-Maaka na Soba.
7 [g]Wakakodisha magari ya vita 32,000
yakiwa na waendeshaji wake, pamoja
na mfalme wa Maaka na vikosi vyake,
wakaja na kupiga kambi karibu na Medeba.
Waamoni nao wakakusanyika toka miji yao,
wakatoka ili kupigana vita.

8 Daudi aliposikia jambo hili, akamtuma
Yoabu na jeshi lote la wapiganaji.
9 Waamoni wakatoka wakajipanga wakiwa
tayari kwa vita langoni la mji wao, wakati
wale wafalme wengine waliokuja nao
walijipanga kwa vita uwanjani.

10 Yoabu akaona kuwa mbele yake na
nyuma yake kumepangwa vita; kwa hiyo
akachagua baadhi ya vikosi vilivyo bora
sana katika Israeli akavipanga dhidi ya
Waaramu. 11 [h]Akawaweka wale wanajeshi
wengine waliobaki chini ya amri ya
Abishai ndugu yake, nao wakapangwa
ili wakabiliane na Waamoni. 12 Yoabu
akasema, “Kama Waaramu watanizidi
nguvu, basi itakupasa wewe unisaidie;
lakini kama Waamoni watakuzidi nguvu,
basi mimi nitakusaidia. 13 [i]Uwe hodari na
tupigane kwa ujasiri kwa ajili ya watu wetu
na miji ya Mungu wetu. BWANA atafanya
lile lililo jema machoni pake.”

14 [j]Basi Yoabu na vikosi vyake wakasonga
mbele kupigana na Waaramu, nao Waaramu
wakakimbia mbele yake. 15 Waamoni
walipoona Waaramu wanakimbia, nao pia
wakakimbia mbele ya nduguye Abishai na
kuingia ndani ya mji. Basi Yoabu akarudi
Yerusalemu.

16 [k]Baada ya Waaramu kuona kwamba
wameshindwa na Israeli, wakapeleka
wajumbe na kuwataka Waaramu wengine
kutoka ng’ambo ya Mto Frati, wakiongozwa
na Shofaki, jemadari wa jeshi la Hadadezeri.

17 Daudi alipoambiwa haya,
akawakusanya Israeli wote na kuvuka
Yordani. Akasonga mbele dhidi yao na
akajipanga kuwakabili. Daudi akapanga vita
ili kupigana na Waaramu, nao wakapigana
dhidi yake. 18 [l]Lakini Waaramu wakakimbia
mbele ya Israeli, naye Daudi akawaua
waendesha magari 7,000 na askari wao
wa miguu 40,000. Pia akamuua Shofaki,
jemadari wa jeshi lao.

19 Raiya wa Hadadezeri walipoona
kuwa wameshindwa na Israeli, wakafanya

---

[a]**19:1** 2Nya 20:1-2; Sef 2:8-11; 2Sam 10:1
[b]**19:3** Hes 21:32
[c]**19:5** 1Fal 16:34; Amu 16:22; Yos 6:24-26
[d]**19:6** Mwa 34:30; 1Nya 18:3; 1Sam 14:47; 2Sam 8:3; 10:6; 1Fal 11:23
[e]6 Talanta 1,000 za fedha ni sawa na tani 34.
[f]6 Yaani Mesopotamia ya Kaskazini-Magharibi.
[g]**19:7** Hes 21:30; Yos 13:9-16; Isa 15:2
[h]**19:11** 1Sam 26:6
[i]**19:13** Isa 30:18; Yer 17:5-8; Za 20:7; 34:22; Mt 16:3, 20
[j]**19:14** Law 26:7-8; Hes 14:9; Kum 28:7
[k]**19:16** 2Sam 10:16
[l]**19:18** Za 33:16; Mit 21:31

mapatano ya amani na Daudi, wakawa
watumishi wake.
Hivyo Waaramu hawakukubali
kuwasaidia Waamoni tena.

*Kutekwa Kwa Raba*

**(2 Samweli 12:26-31)**

20 [a]Mwanzoni mwa mwaka mpya, wakati
ambapo wafalme huenda vitani, Yoabu
aliliongoza jeshi. Aliangamiza nchi ya
Waamoni, na akaenda Raba na kuuzingira,
lakini Daudi alibaki Yerusalemu. Yoabu
akashambulia Raba na kuuacha ukiwa
magofu. 2 [b]Daudi akachukua taji kutoka
kwa kichwa cha mfalme wao, lililokuwa
na uzito wa talanta moja ya dhahabu,[c] nayo
ilizungushiwa vito vya thamani. Ikawekwa
juu ya kichwa cha Daudi. Alichukua nyara
nyingi kutoka mjini huo. 3 [d]Akawatoa watu
waliokuwa humo, akawaweka wafanye
kazi kwa misumeno, sululu za chuma na
mashoka. Daudi akafanya hivi kwa miji
yote ya Waamoni. Kisha Daudi na jeshi
lake lote wakarudi Yerusalemu.

*Vita Na Wafilisti*

**(2 Samweli 21:15-22)**

4 [e]Baada ya muda, kulitokea vita dhidi ya
Wafilisti, huko Gezeri. Wakati huo Sibekai,
Mhushathi, akamuua Sipai, aliyekuwa
mmoja wa wazao wa Warefai,[f] nao Wafilisti
wakashindwa.
5 [g]Katika vita vingine na Wafilisti,
Elhanani mwana wa Yairi alimuua Lahmi
nduguye Goliathi, Mgiti, ambaye mkuki
wake ulikuwa na mpini kama mti wa
mfumaji.
6 Katika vita vingine tena, vilivyopiganwa
huko Gathi, kulikuwako na mtu mmoja
mkubwa mwenye vidole sita katika kila
mkono na vidole sita katika kila mguu:
jumla vidole ishirini na vinne. Yeye alikuwa
pia mzao wa Mrefai. 7 Alipowadhihaki
Israeli, Yonathani, mwana wa Shimea,
nduguye Daudi, akamuua.
8 Hawa walikuwa ndio wazao wa Warefai
huko Gathi, nao walianguka kwa mikono
ya Daudi na watu wake.

*Daudi Ahesabu Wapiganaji*

**(2 Samweli 24:1-25)**

21 [h]Shetani akainuka dhidi ya Israeli na
kumshawishi Daudi ahesabu watu wa
Israeli. 2 [i]Kwa hiyo Daudi akamwambia
Yoabu na majemadari wa jeshi, "Nendeni
mkawahesabu Waisraeli kuanzia Beer-
Sheba mpaka Dani. Kisha nileteeni taarifa ili
kwamba niweze kufahamu wako wangapi."
3 Yoabu akajibu, "BWANA na aongeze
jeshi lake mara mia na zaidi. Mfalme bwana
wangu, kwani hawa wote si raiya wa bwana
wangu? Kwa nini bwana wangu unataka
kufanya hivi? Kwa nini kuleta hatia juu
ya Israeli?"
4 [j]Hata hivyo, neno la mfalme likawa
na nguvu juu ya Yoabu; kwa hiyo Yoabu
akaondoka na kuzunguka Israeli yote kisha
akarudi Yerusalemu. 5 Yoabu akampa
Daudi jumla ya idadi ya watu wanaoweza
kupigana. Katika Israeli kulikuwa na watu
1,100,000 ambao wangeweza kutumia
upanga na katika Yuda watu 470,000.
6 [k]Lakini Yoabu hakuwahesabu Walawi
na Wabenyamini, kwa sababu alichukizwa
sana na amri ya mfalme. 7 Amri hii ilikuwa
mbaya machoni pa Mungu pia; hivyo
akaiadhibu Israeli.
8 [l]Kisha Daudi akamwambia Mungu,
"Nimetenda dhambi kubwa kwa kufanya
jambo hili. Sasa, ninakusihi, ondoa hatia
ya mtumishi wako. Nimefanya jambo la
kipumbavu sana."

---

[a]**20:1** Kum 3:11; 2Sam 12:26; Amo 1:13-15; 2Nya 36:10; Mhu 3:8; Yer 49:2; 1Sam 11:1; 1Fal 20:22; Eze 21:20
[b]**20:2** 2Sam 12:30-31
[c]2 Talanta moja ya dhahabu ni sawa na kilo 34.
[d]**20:3** Kum 29:11
[e]**20:4** Yos 10:33; Mwa 14:5
[f]4 Yaani majitu.
[g]**20:5** 1Sam 17:7
[h]**21:1** 2Nya 18:21; 1Fal 22:20-22; Za 109:6; 2Nya 14:8; Ufu 12:9; 2Nya 25:5; Mt 4:2; Yn 13:2; Mdo 5:3
[i]**21:2** 1Nya 27:23-24
[j]**21:4** Mit 29:25; Mdo 5:29; 4:19; Mhu 8:4
[k]**21:6** Hes 1:47-49; 1Nya 27:24
[l]**21:8** 2Sam 24:10; Ay 42:6; Hos 14:2; Za 25:11; 51:1-3; Mit 28:13-14; 2Kor 7:10

9 [a]BWANA akamwambia Gadi, mwonaji wa
Daudi, 10 "Nenda ukamwambie Daudi, hivi
ndivyo asemavyo Bwana: 'Ninakupa wewe
uchaguzi wa mambo matatu. Nichagulie
mojawapo nitakalotenda dhidi yako.' "
11 Kwa hiyo Gadi akamwendea Daudi
akamwambia, "Hili ndilo BWANA asemalo:
'Chagua: 12 [b]miaka mitatu ya njaa, au
miezi mitatu ya kushindwa na adui zako,
ukipatwa na upanga wao, au siku tatu za
upanga wa BWANA, yaani, siku tatu za
tauni katika nchi na malaika wa BWANA
akiangamiza kila mahali katika Israeli.'
Sasa basi, amua jinsi nitakavyomjibu yeye
aliyenituma."
13 [c]Daudi akamwambia Gadi, "Ninayo
mahangaiko makubwa. Mimi na nianguke
mikononi mwa BWANA kwa maana rehema
zake ni kuu mno, lakini usiniache niangukie
mikononi mwa wanadamu."
14 [d]Basi BWANA akatuma tauni katika
Israeli, watu 70,000 wa Israeli wakafa.
15 [e]Mungu akapeleka malaika kuangamiza
Yerusalemu. Lakini malaika alipokuwa
akifanya hivyo, BWANA akaona na
akahuzunika kwa sababu ya maafa,
akamwambia yule malaika aliyekuwa
anaangamiza watu, "Yatosha! Rudisha
mkono wako." Wakati huo malaika wa
BWANA alikuwa amesimama katika sakafu
ya kupuria nafaka ya Arauna[f] Myebusi.
16 [g]Daudi akayainua macho yake
akamwona huyo malaika wa BWANA akiwa
amesimama katikati ya mbingu na dunia,
naye ameunyoosha upanga wake juu ya
Yerusalemu tayari kuangamiza. Kisha
Daudi na wazee, waliokuwa wamevaa nguo
za gunia, wakaanguka kifudifudi.
17 [h]Daudi akamwambia Mungu, "Je, si
mimi ndiye niliyeamuru watu wahesabiwe?
Mimi ndiye niliyetenda dhambi na kukosa.
Hawa ni kondoo tu. Wamefanya nini? Ee
BWANA, Mungu wangu, mkono wako na
uwe juu yangu mimi na jamaa yangu,
lakini usiache tauni hii iendelee juu ya
watu wako."
18 Kisha malaika wa BWANA akamwamuru
Gadi amwambie Daudi apande na
kumjengea BWANA madhabahu kwenye
sakafu ya kupuria nafaka ya Arauna
Myebusi. 19 Kwa hiyo Daudi akakwea,
akalitii lile neno ambalo Gadi alikuwa
amelisema katika jina la BWANA.
20 [i]Arauna alipokuwa akipura ngano,
akageuka akamwona yule malaika. Wanawe
wanne waliokuwa pamoja naye wakajificha,
yeye akaendelea kupura ngano. 21 Kisha
Daudi akakaribia, Arauna alipotazama
na kumwona, akaondoka kwenye uwanja
wa kupuria nafaka akamsujudia Daudi
akiuinamisha uso wake ardhini.
22 [j]Daudi akamwambia, "Nipatie huu
uwanja wako wa kupuria nafaka ili niweze
kujenga madhabahu ya BWANA tauni ipate
kukomeshwa katika watu. Niuzie kwa bei
yake kamili."
23 Arauna akamwambia Daudi, "Uchukue
huo uwanja. Mfalme bwana wangu na
afanye lolote analopenda. Tazama, nitatoa
maksai kwa ajili ya sadaka za kuteketezwa,
vifaa vya kupuria kuwa kuni, pamoja na
ngano kwa ajili ya dhabihu ya nafaka.
Natoa hivi vyote."
24 Lakini Mfalme Daudi akamjibu Arauna,
"La hasha! Lakini ninasisitiza kwamba
nitalipa bei yake kamili. Sitachukua kilicho
chako kwa ajili ya BWANA au kutoa sadaka
ya kuteketezwa ambayo hainigharimu
chochote."
25 [k]Basi Daudi akamlipa Arauna shekeli
za dhahabu 600[l] kwa ajili ya ule uwanja.
26 [m]Kisha Daudi akamjengea BWANA
madhabahu mahali hapo, na kutoa sadaka
za kuteketezwa na sadaka za amani.

[a]**21:9** 1Sam 22:5; 9:9
[b]**21:12** Kum 32:24; Eze 30:25; Mwa 19:13; 2Sam 24:13
[c]**21:13** Neh 9:17; Za 6:4; 130:4-7; Mao 3:22; Za 100:5; 145:9; Yoe 2:13
[d]**21:14** 1Nya 27:24
[e]**21:15** Mwa 32:1; 2Sam 24:16; Mwa 6:6; Kut 32:14; Mwa 19:13; Yer 26:18; Mt 23:37-38; Amu 2:18
[f]15 Pia anaitwa Ornani kwa Kiebrania.
[g]**21:16** Hes 14:5; Yos 7:6; 2Nya 3:1
[h]**21:17** 2Sam 7:8; Za 74:1; Yon 1:12
[i]**21:20** Amu 6:11
[j]**21:22** Hes 16:48; 25:8
[k]**21:25** 2Sam 24:24
[l]25 Shekeli 600 za dhahabu ni sawa na kilo 7.
[m]**21:26** Kut 19:18; 2Nya 7:1

Akamwita BWANA naye BWANA akajibu
maombi yake kwa moto toka mbinguni juu
ya madhabahu ya sadaka ya kuteketezwa.
27 Kisha BWANA akanena na yule malaika,
naye akarudisha upanga wake katika
ala yake. 28 Wakati huo, Daudi alipoona
kwamba BWANA amemjibu kule kwenye
uwanja wa kupuria nafaka wa Arauna
Myebusi, akatoa dhabihu huko. 29 [a]Maskani
ya BWANA ambayo Mose aliitengeneza
kule jangwani, pamoja na madhabahu ya
sadaka ya kuteketezwa kwa wakati huo
vilikuwa viko mahali pa juu pa kuabudia
huko Gibeoni. 30 [b]Lakini Daudi hakuthubutu
kuisogelea ili kumuuliza Mungu, kwa
sababu aliuogopa upanga wa yule malaika
wa BWANA.

22 [c]Ndipo Daudi akasema, "Nyumba ya
BWANA Mungu itakuwa mahali hapa,
pia pamoja na madhabahu ya sadaka ya
kuteketezwa kwa ajili ya Israeli."

### *Maandalizi Kwa Ajili Ya Hekalu*

2 [d]Kwa hiyo Daudi akatoa amri
wakusanyike wageni wote waliokuwa
wanaishi Israeli, na kutoka miongoni
mwao akaweka waashi ili kuchonga mawe
kwa ajili ya kujenga nyumba ya Mungu.
3 [e]Daudi akatoa chuma tele ili kutengenezea
misumari kwa ajili ya mafungo ya malango
ya nyumba na shaba tele isiyopimika. 4 [f]Pia
akatoa magogo ya mierezi yasiyohesabika,
kwa kuwa Wasidoni na Watiro walikuwa
wamemletea Daudi idadi kubwa ya mierezi.
5 [g]Daudi akasema, "Mwanangu Solomoni
bado ni mdogo wa umri na hana uzoefu.
Nyumba itakayojengwa kwa ajili ya BWANA
inatakiwa iwe yenye uzuri mwingi na sifa
na fahari mbele ya mataifa yote. Kwa hiyo
nitaifanyia matayarisho." Daudi akafanya
matayarisho makubwa kabla ya kifo chake.
6 [h]Kisha akamwita Solomoni mwanawe
akamwagiza kujenga nyumba kwa ajili
ya BWANA, Mungu wa Israeli. 7 [i]Daudi
akamwambia Solomoni: "Mwanangu,
nilikuwa na jambo hili ndani ya moyo
wangu kujenga nyumba kwa ajili ya Jina
la BWANA Mungu wangu. 8 [j]Lakini neno
hili la BWANA likanijia, kusema: 'Wewe
umemwaga damu nyingi na kupigana vita
vingi. Wewe hutajenga nyumba kwa ajili ya
Jina langu, kwa sababu umemwaga damu
nyingi juu ya nchi machoni pangu. 9 [k]Lakini
utakuwa na mwana ambaye atakuwa mtu
wa amani na utulivu nami nitampa utulivu
mbele ya adui zake wote pande zote. Jina
lake ataitwa Solomoni, nami nitawapa
Israeli amani na utulivu wakati wa utawala
wake. 10 [l]Yeye ndiye atakayejenga nyumba
kwa ajili ya Jina langu. Yeye atakuwa
mwanangu, nami nitakuwa baba yake.
Nami nitakifanya imara kiti chake cha enzi
cha utawala wake katika Israeli milele.'
11 [m]"Sasa, mwanangu, BWANA awe
pamoja nawe, nawe uwe na mafanikio upate
kuijenga nyumba ya BWANA Mungu wako,
kama alivyosema utafanya. 12 [n]BWANA
na akupe hekima na ufahamu wakati
atakuweka juu ya Israeli, ili uweze kuishika
sheria ya BWANA Mungu wako. 13 [o]Ndipo
utakapofanikiwa, ikiwa utakuwa na bidii
kutii amri na sheria BWANA alizompa Mose
kwa ajili ya Israeli. Uwe hodari na ushujaa.
Usiogope wala usikate tamaa.
14 [p]"Nimejitaabisha sana ili kupata
mahitaji kwa ajili ya Hekalu la BWANA:
talanta 100,000[q] za dhahabu, talanta

---

[a]**21:29** Yos 9:3; 1Fal 3:4; 1Nya 16:39
[b]**21:30** 1Nya 13:12; Ay 13:21; 2Sam 6:9; Ay 21:6; Za 119:120
[c]**22:1** Kum 12:5; Mwa 28:17; 1Nya 21:18-28; 2Nya 3:1; Kum 12:5; 2Sam 24:18
[d]**22:2** Kum 20:11; 1Fal 9:21; 5:17-18; Ezr 3:7
[e]**22:3** 1Fal 7:47
[f]**22:4** 1Fal 5:6
[g]**22:5** 1Fal 3:7; 1Nya 29:1
[h]**22:6** Mdo 7:47
[i]**22:7** 1Nya 17:2; 2Sam 7:2; 1Fal 8:17; Kum 12:5-11; Mdo 7:48
[j]**22:8** 1Fal 5:3; 1Nya 28:3
[k]**22:9** Yos 14:15; 2Sam 12:24; 1Fal 4:20; 5:4; 1Nya 28:5
[l]**22:10** 1Nya 17:12; 2Sam 7:13-14; 2Nya 6:15; 1Fal 5:5; 1Nya 28:6; Za 89:26-27; Ebr 1:5
[m]**22:11** 1Sam 18:12; Rum 8:31
[n]**22:12** 1Fal 3:11; 2Nya 1:10; Kum 4:6
[o]**22:13** 1Nya 28:7; Kum 31:6-7; Yos 1:6-9; 1Fal 6:12-13; 9:4-5; Isa 3:10; 1Nya 28:20
[p]**22:14** 1Nya 29:2-5, 19
[q]14 Talanta 100,000 za dhahabu ni sawa na tani 3,750.

1,000,000[a] za fedha na kiasi kisichopimika
cha shaba na chuma, pia mbao na mawe.
Nawe waweza kuviongeza. 15 Unao
wafanyakazi wengi: Wachonga mawe,
waashi na maseremala, pamoja na watu
walio na ustadi katika kila kazi 16 wa kufua
dhahabu, fedha, shaba na chuma, mafundi
wasiohesabika. Sasa basi anza kazi hii, naye
BWANA awe pamoja nawe."
17 [b]Kisha Daudi akawaamuru viongozi
wote wa Israeli wamsaidie Solomoni
mwanawe. 18 [c]Akawaambia, "Je, BWANA
Mungu wenu si yuko pamoja na ninyi?
Pia si amewapa raha pande zote? Kwa
maana amewatia wenyeji wa nchi mkononi
mwangu, nayo nchi iko chini ya BWANA
na watu wake. 19 [d]Sasa itoeni mioyo yenu
na nafsi zenu katika kumtafuta BWANA
Mungu wenu. Anzeni kujenga Maskani ya
BWANA Mungu, ili mweze kulileta Sanduku
la Agano la BWANA na vyombo vitakatifu
vya Mungu katika Hekalu litakalojengwa
kwa ajili ya Jina la BWANA."

*Jamaa Za Walawi Na Utendaji Wao*

23 [e]Daudi alipokuwa mzee aliyeshiba
siku, akamfanya Solomoni mwanawe
kuwa mfalme juu ya Israeli.
2 Pia akawakusanya pamoja viongozi
wote wa Israeli, pamoja na makuhani na
Walawi. 3 [f]Walawi waliokuwa na umri wa
miaka thelathini au zaidi walihesabiwa,
nayo hesabu ya wanaume ilikuwa 38,000.
4 [g]Daudi akasema, "Miongoni mwa hawa,
24,000 watasimamia kazi ya Hekalu la
BWANA na 6,000 watakuwa maafisa na
waamuzi, 5 [h]na 4,000 watakuwa mabawabu,
na wengine 4,000 watamsifu BWANA kwa
ala za uimbaji nilizotoa kwa ajili ya kusudi
hilo."
6 [i]Daudi akawagawa Walawi katika
makundi kufuatana na wana wa Lawi:
Gershoni, Kohathi na Merari.

*Wagershoni*

7 Wana wa Wagershoni walikuwa
wawili:
Ladani na Shimei.
8 Wana wa Ladani walikuwa watatu:
Yehieli wa kwanza, Zethamu na
Yoeli.
9 Wana wa Shimei walikuwa watatu:
Shelomothi,[j] Hazieli na Harani.
Hawa watatu walikuwa viongozi
wa jamaa za Ladani.
10 Nao wana wa Shimei walikuwa
wanne:
Yahathi, Zina,[k] Yeushi na Beria.
11 Yahathi alikuwa wa kwanza na
Ziza wa pili, lakini Yeushi na Beria
hawakuwa na wana wengi; kwa
hiyo walihesabiwa kama jamaa
moja, wakapewa wajibu kwa
pamoja.

*Wakohathi*

12 [l]Wana wa Kohathi walikuwa wanne:
Amramu, Ishari, Hebroni na
Uzieli.
13 [m]Wana wa Amramu walikuwa:
Aroni na Mose.
Aroni waliwekwa wakfu, yeye
na wazao wake milele, wawe
wakiweka wakfu vitu ambavyo
ni vitakatifu mno, kutoa dhabihu
mbele za BWANA, kuhudumu
mbele zake na kutamka baraka
katika Jina la BWANA milele.
14 [n]Wana wa Mose mtu wa Mungu

---

[a]14 Talanta 1,000,000 za fedha ni sawa na tani 37,500.
[b]**22:17** 1Nya 28:1-6
[c]**22:18** 1Fal 8:6; Kum 12:10; Yos 22:4
[d]**22:19** 2Nya 20:3; 1Fal 8:6; 2Nya 5:7; 6:11
[e]**23:1** 1Fal 1:30-33; 1Nya 28:5; 29:28; 29:22-25
[f]**23:3** Hes 8:24; 4:3-49
[g]**23:4** Ezr 3:8; 2Nya 19:8; Kum 16:18; Eze 44:24; Kum 16:18; 1Nya 26:29
[h]**23:5** 1Nya 15:16; Za 92:3; Neh 12:45; Amo 6:5; 2Nya 29:25-26
[i]**23:6** 2Nya 23:18; 29:25; 8:14; Kut 6:16; Hes 26:57; 2Nya 35:10; 31:2; Ezr 6:18
[j]9 Yaani Shelomithi; maana yake ni Mpenda amani.
[k]10 Tafsiri zingine zinamwita Ziza.
[l]**23:12** Mwa 46:11; Kut 6:18-20; 1Nya 6:2
[m]**23:13** Kut 30:7-10; 28:1; Kum 21:5; Hes 6:23; 16:40; Ebr 5:4; Hes 16:40; 1Sam 2:28
[n]**23:14** Kum 33:1

walihesabiwa kama sehemu ya
kabila la Lawi.
15 [a]Wana wa Mose walikuwa:
Gershomu na Eliezeri.
16 [b]Wazao wa Gershomu:
Shebueli alikuwa wa kwanza.
17 Wazao wa Eliezeri:
Rehabia alikuwa wa kwanza.
Eliezeri alikuwa na mwana mmoja
tu, lakini wana wa Rehabia
walikuwa wengi sana.
18 Wana wa Ishari:
Shelomithi alikuwa wa kwanza.
19 [c]Wana wa Hebroni walikuwa:
Yeria alikuwa wa kwanza, wa pili
Amaria, wa tatu Yahazieli, na wa
nne Yekameamu.
20 Wana wa Uzieli walikuwa:
Mika wa kwanza na Ishia wa pili.

*Wamerari*

21 [d]Wana wa Merari walikuwa:
Mahli na Mushi.
Wana wa Mahli walikuwa:
Eleazari na Kishi.
22 [e]Eleazari akafa bila ya kuwa na
wana: alikuwa na binti tu. Binamu
zao, wana wa Kishi, wakawaoa.
23 [f]Wana wa Mushi:
Mahli, Ederi na Yeremothi; wote
walikuwa watatu.

24 [g]Hawa walikuwa wazao wa Lawi
kwa jamaa zao. Wakuu wa jamaa kama
walivyoandikwa kwa majina yao na
kuhesabiwa kila mmoja, yaani, wenye
uwezo wa kufanya kazi kuanzia miaka
ishirini au zaidi, waliohudumu katika
Hekalu la Bwana.
25 Kwa maana Daudi
alikuwa amesema, "Kwa vile Bwana,
Mungu wa Israeli amewapa watu wake
raha na amekuja kuishi Yerusalemu milele,
26 Walawi hawahitaji tena kubeba Maskani
wala chombo chochote cha utumishi wake."
27 Kulingana na maagizo ya mwisho ya
Daudi, Walawi waliohesabiwa ni wale wa
kuanzia umri wa miaka ishirini au zaidi.
28 [h]Wajibu wa Walawi ulikuwa kuwasaidia
wazao wa Aroni kuhudumu katika Hekalu
la Bwana: Kuwa wasimamizi wa nyua,
vyumba vya pembeni, kutakasa vyombo
vitakatifu na utendaji mwingine wowote
katika nyumba ya Mungu.
29 [i]Walikuwa
wasimamizi wa mikate iliyowekwa mezani,
unga kwa ajili ya sadaka za nafaka, mikate
isiyotiwa chachu, uokaji na uchanganyaji,
pamoja na vipimo vyote vya wingi na
ukubwa.
30 [j]Pia ulikuwa wajibu wao kila
asubuhi kumshukuru na kumsifu Bwana.
Iliwapasa pia kufanya hivyo jioni
31 [k]na
wakati wowote sadaka za kuteketezwa
zilipotolewa kwa Bwana siku za Sabato
na kwenye sikukuu za Mwezi Mwandamo
na katika sikukuu nyingine zilizoamriwa.
Iliwapasa kuhudumu mbele za Bwana
mara kwa mara kwa idadi maalum na kwa
namna waliyokuwa wamepewa maelekezo.
32 [l]Hivyo Walawi wakafanya wajibu wao
katika Hema la Kukutania, katika Mahali
Patakatifu chini ya uongozi wa ndugu zao
wazao wa Aroni, kwa ajili ya utumishi
katika Hekalu la Bwana.

*Migawanyo Ya Makuhani*

24 [m]Hii ndiyo migawanyo ya wana wa
Aroni:
Aroni alikuwa na wana wanne: Nadabu,
Abihu, Eleazari na Ithamari.
2 [n]Nadabu na
Abihu walikufa kabla ya baba yao, nao
hawakuwa na wana; kwa hiyo ndugu
zao Eleazari na Ithamari wakahudumu
kama makuhani.
3 [o]Akisaidiwa na Sadoki

[a]**23:15** Kut 18:4; 2:22
[b]**23:16** 1Nya 26:24-28
[c]**23:19** 1Nya 24:23; 26:31
[d]**23:21** 1Nya 6:19; 24:26
[e]**23:22** Hes 36:6
[f]**23:23** 1Nya 24:30
[g]**23:24** Hes 4:3; 10:17-21
[h]**23:28** Neh 13:9; Mal 3:3
[i]**23:29** Kut 25:30; Law 2:4-7; 6:20-23; 19:35-36; 1Nya 9:29-32
[j]**23:30** 1Nya 9:33; Ufu 5:8-14; 2Nya 31:2; 1Nya 6:31-33; Za 135:1-3; Ufu 14:3
[k]**23:31** 2Fal 4:23; Law 23:4; Kol 2:16; Hes 10:10; Za 81:3; Isa 1:13-14
[l]**23:32** Hes 1:53; 1Nya 6:48; Hes 3:6-8; 2Nya 31:2; Eze 44:14
[m]**24:1** 2Nya 5:11; Ezr 6:18; Kut 6:23; Hes 3:2-4; 26:60
[n]**24:2** Law 10:1-2; Hes 3:4; 26:61
[o]**24:3** 2Sam 8:17

mwana wa Eleazari na Ahimeleki mwana
wa Ithamari, Daudi aliwapanga wazao
wa Aroni katika migawanyo kufuatana
na wajibu wa huduma zao. 4 Idadi kubwa
ya viongozi walipatikana miongoni mwa
wazao wa Eleazari, kuliko miongoni mwa
wazao wa Ithamari, nao waligawanywa
kwa uwiano: Viongozi kumi na sita kutoka
jamaa ya wazao wa Eleazari na viongozi
wanane kutoka jamaa ya wazao wa
Ithamari. 5 [a]Waliwagawanya bila upendeleo
kwa kupiga kura, kwa kuwa kulikuwa na
maafisa wa mahali patakatifu na maafisa
wa Mungu miongoni mwa wazao wale wa
Eleazari na wale wa Ithamari.

6 [b]Mwandishi Shemaya mwana wa
Nethaneli, Mlawi, aliorodhesha majina yao
mbele ya Mfalme Daudi na maafisa: Kuhani
Sadoki, Ahimeleki mwana wa Abiathari,
na viongozi wa jamaa za makuhani na za
Walawi: jamaa moja ikitoka upande wa
Eleazari na nyingine upande wa Ithamari.

7 [c]Kura ya kwanza ilimwangukia
Yehoyaribu,
ya pili Yedaya,
8 [d]ya tatu Harimu,
ya nne Seorimu,
9 ya tano Malkiya,
ya sita Miyamini,
10 [e]ya saba Hakosi,
ya nane Abiya,
11 ya tisa Yeshua,
ya kumi Shekania,
12 ya kumi na moja Eliashibu,
ya kumi na mbili Yakimu,
13 ya kumi na tatu Hupa,
ya kumi na nne Yeshebeabu,
14 [f]ya kumi na tano Bilga,
ya kumi na sita Imeri,
15 [g]ya kumi na saba Heziri,
ya kumi na nane Hapisesi,
16 ya kumi na tisa Pethahia,
ya ishirini Yehezkeli,
17 ya ishirini na moja Yakini,
ya ishirini na mbili Gamuli,
18 ya ishirini na tatu Delaya,
ya ishirini na nne Maazia.

19 [h]Huu ulikuwa ndio utaratibu wao
uliokubalika wa kuhudumu walipoingia
katika Hekalu la Bwana kulingana na
masharti waliyoelekezwa na Aroni baba
yao, kama Bwana, Mungu wa Israeli,
alivyokuwa amemwamuru.

### *Walawi Waliobaki*

20 [i]Kuhusu wazao wa Lawi waliobaki:

Kutoka kwa wana wa Amramu:
alikuwa Shubaeli;
kutoka kwa wana wa Shubaeli:
alikuwa Yedeya.
21 Kwa wa Rehabia, kutoka kwa
wanawe:
Ishia alikuwa wa kwanza.
22 Kutoka kwa Waishari: alikuwa
Shelomithi,
kutoka kwa wana wa Shelomithi:
alikuwa Yahathi.
23 [j]Wana wa Hebroni: Yeria alikuwa
mkuu, Amaria wa pili, Yahazieli
wa tatu, na Yekameamu wa nne.
24 Mwana wa Uzieli: alikuwa Mika;
kutoka kwa wana wa Mika:
alikuwa Shamiri.
25 [k]Ndugu yake Mika: alikuwa Ishia;
na kutoka kwa wana wa Ishia:
alikuwa Zekaria.
26 [l]Wana wa Merari: walikuwa Mahli
na Mushi.
Mwana wa Yaazia: alikuwa Beno.
27 Wana wa Merari:
kutoka kwa Yaazia: ni Beno,
Shohamu, Zakuri na Ibri.
28 [m]Kutoka kwa Mahli: alikuwa

[a]**24:5** 1Nya 26:13; Mdo 1:26; Yos 18:10; Mit 16:33; 18:18
[b]**24:6** 1Nya 18:16; Neh 8:4; 1Fal 4:3
[c]**24:7** Ezr 2:36; Neh 7:39; 12:6
[d]**24:8** Ezr 10:21; Neh 12:4-6
[e]**24:10** Neh 12:4, 17; Lk 1:5
[f]**24:14** Ezr 2:37; Yer 20:1
[g]**24:15** Neh 10:20
[h]**24:19** 1Nya 9:25; Hes 4:49; 2Fal 5:7; Lk 1:18-23
[i]**24:20** 1Nya 23:6-17
[j]**24:23** 1Nya 23:19; 15:9
[k]**24:25** 1Nya 22:9
[l]**24:26** 1Nya 6:19; 23:21; Hes 3:20; Kut 6:19
[m]**24:28** 1Nya 23:22

Eleazari, ambaye hakuwa na
wana.
29 Kutoka kwa Kishi: mwana wa Kishi:
alikuwa Yerameeli.
30 [a]Nao wana wa Mushi: walikuwa
Mahli, Ederi na Yeremothi.

Hawa walikuwa Walawi kulingana na
jamaa zao. 31 Pia walipiga kura kama vile
ndugu zao wazao wa Aroni walivyofanya,
mbele ya Mfalme Daudi, Sadoki, Ahimeleki
na mbele ya viongozi wa jamaa ya makuhani
na ya Walawi. Jamaa za ndugu wakubwa
zilitendewa sawasawa na zile za ndugu
wadogo.

*Waimbaji*

25 [b]Daudi, pamoja na majemadari wa
jeshi, wakakawatenga baadhi ya wana
wa Asafu, wana wa Hemani na wana wa
Yeduthuni, kwa ajili ya huduma ya kutoa
unabii, wakitumia vinubi, zeze na matoazi.
Hii ndiyo orodha ya watu waliofanya
huduma hii:

2 Kutoka kwa wana wa Asafu
walikuwa:
Zakuri, Yosefu, Nethania na
Asarela. Wana wa Asafu walikuwa
chini ya usimamizi wa Asafu,
ambaye alitoa unabii chini ya
usimamizi wa mfalme.
3 [c]Wana wa Yeduthuni walikuwa sita:
Gedalia, Seri, Yeshaya, Shimei,
Hashabia, na Matithia, nao
walikuwa chini ya usimamizi
wa baba yao Yeduthuni, wao
walikuwa wakitoa unabii
wakitumia vinubi, wakimshukuru
na kumtukuza Bwana.
4 Wana wa Hemani walikuwa:
Bukia, Matania, Uzieli, Shebueli
na Yeremothi, Hanania, Hanani,
Eliatha, Gidalti na Romamti-
Ezeri, Yoshbekasha, Malothi,
Hothiri na Mahaziothi. 5 [d]Wote
hawa walikuwa wana wa Hemani
mwonaji wa mfalme. Aliwapata
wana hawa kutokana na ahadi
ya Mungu ili kumwinua. Mungu
alimpa Hemani wana kumi na
wanne na binti watatu.

6 [e]Hawa wanaume wote walikuwa chini
ya usimamizi wa baba yao kwa ajili ya
uimbaji katika Hekalu la Bwana wakitumia
matoazi, zeze na vinubi, kwa ajili ya
huduma katika nyumba ya Mungu. Asafu,
Yeduthuni na Hemani walikuwa chini ya
usimamizi wa mfalme. 7 [f]Pamoja na ndugu
zao wote walikuwa wamefundishwa na
kuwa stadi wa uimbaji kwa Bwana. Idadi
yao walikuwa 288. 8 [g]Vijana kwa wazee,
walimu kwa wanafunzi, wote walipanga
kazi zao kwa kupiga kura.

9 [h]Kura ya kwanza, ambayo ilikuwa
kwa ajili ya Asafu, ilimwangukia
Yosefu, wanawe na jamaa zake, 12
Ya pili ikamwangukia Gedalia, yeye
na wanawe pamoja na jamaa zake,
12
10 Ya tatu ikamwangukia Zakuri,
wanawe na jamaa zake, 12
11 ya nne ikamwangukia Isri,[i] wanawe
na jamaa zake, 12
12 ya tano ikamwangukia Nethania,
wanawe na jamaa zake, 12
13 ya sita ikamwangukia Bukia,
wanawe na jamaa zake, 12
14 ya saba ikamwangukia Yesarela,[j]
wanawe na jamaa zake, 12
15 ya nane ikamwangukia Yeshaya,
wanawe na jamaa zake, 12
16 ya tisa ikamwangukia Matania,
wanawe na jamaa zake, 12

---

[a]**24:30** 1Nya 23:23
[b]**25:1** 1Nya 6:31-39; 16:41-42; Neh 11:17; 1Sam 10:5; Ezr 3:10; 2Nya 5:12; 1Nya 12:28; 23:2; 15:17; Kut 15:20; Hes 11:25; Za 150:3-5; 1Kor 14:1; Ufu 15:2-4
[c]**25:3** Mwa 4:21; Za 33:2
[d]**25:5** 1Sam 9:9; 2Sam 24:11; Amo 7:12; 1Pet 4:11; Isa 3:18; 1Nya 21:9; 26:28; Mwa 33:5; 1Sam 1:17; 1Nya 28:5; Za 127:3; 128:3
[e]**25:6** 1Nya 15:16-19; 2Nya 23:18; 29:25
[f]**25:7** Efe 5:19; Kol 3:16; Yak 5:13
[g]**25:8** 2Nya 23:13; 1Nya 26:13
[h]**25:9** 1Nya 6:36-39; 25:31; Ufu 5:8; 1Nya 9:33
[i]11 Isri jina lingine ni Seri.
[j]14 Yesarela jina lingine ni Asarela.

17 ya kumi ikamwangukia Shimei, wanawe na jamaa zake, 12
18 ya kumi na moja ikamwangukia Azareli,[a] wanawe na jamaa zake, 12
19 ya kumi na mbili ikamwangukia Hashabia, wanawe na jamaa zake, 12
20 ya kumi na tatu ikamwangukia Shubaeli, wanawe na jamaa zake, 12
21 ya kumi na nne ikamwangukia Matithia, wanawe na jamaa zake, 12
22 ya kumi na tano ikamwangukia Yeremothi, wanawe na jamaa zake, 12
23 Ya kumi na sita ikamwangukia Hanania, wanawe na jamaa zake, 12
24 ya kumi na saba ikamwangukia Yoshbekasha, wanawe na jamaa zake, 12
25 ya kumi na nane ikamwangukia Hanani, wanawe na jamaa zake, 12
26 ya kumi na tisa ikamwangukia Malothi, wanawe na jamaa zake, 12
27 ya ishirini ikamwangukia Eliatha, wanawe na jamaa zake, 12
28 ya ishirini na moja ikamwangukia Hothiri, wanawe na jamaa zake, 12
29 ya ishirini na mbili ikamwangukia Gidalti, wanawe na jamaa zake, 12
30 ya ishirini na tatu ikamwangukia Mahaziothi, wanawe na jamaa zake, 12
31 [b]ya ishirini na nne ikamwangukia Romamti-Ezeri, wanawe na jamaa zake, 12.

[a]18 Azareli jina lingine ni Uzieli.
[b]**25:31** Ufu 4:4; 5:8; 11:6

*Mabawabu*

26 [c]Hii ndiyo migawanyo ya mabawabu:

Kutoka kwa wana wa Kora alikuwa: Meshelemia mwana wa Kore, mmoja wa wana wa Asafu.
2 [d]Meshelemia alikuwa na wana wafuatao:
Zekaria mzaliwa wa kwanza,
Yediaeli wa pili,
Zebadia wa tatu,
Yathnieli wa nne,
3 Elamu wa tano
Yehohanani wa sita
na Eliehoenai wa saba.
4 Obed-Edomu naye alikuwa na wana wafuatao:
Shemaya mzaliwa wa kwanza,
Yehozabadi wa pili,
Yoa wa tatu,
Sakari wa nne,
Nethaneli wa tano,
5 [e]Amieli wa sita,
Isakari wa saba,
na Peulethai wa nane.
(Kwa kuwa Mungu alikuwa amembariki Obed-Edomu.)

6 Shemaya mwanawe pia alikuwa na wana, waliokuwa viongozi katika jamaa ya baba yao kwa sababu walikuwa watu wenye uwezo
mkubwa. 7 Wana wa Shemaya ni: Othni, Refaeli, Obedi na Elizabadi; jamaa zake Elihu na Semakia walikuwa pia watu wenye uwezo.
8 Hawa wote walikuwa wazao wa Obed-Edomu; wao na wana wao na jamaa zao walikuwa watu wenye uwezo pamoja na nguvu za kufanya kazi. Wazao wa Obed-Edomu jumla yao walikuwa sitini na wawili.
9 Meshelemia alikuwa na wana na jamaa zake, waliokuwa watu

[c]**26:1** 1Nya 9:17; Hes 26:9-11; 2Nya 23:19; Hes 16:1-2; 1Nya 15:18; Yud 11; 1Nya 6:39
[d]**26:2** 1Nya 9:21
[e]**26:5** Mwa 33; 5; 2Sam 5:10; 1Nya 13:13-14; Za 127:3

wenye uwezo: jumla yao watu
kumi na wanane.

10 [a]Hosa, Mmerari, alikuwa na wana
wafuatao: Shimri alikuwa
mkuu wao (baba yake alikuwa
amemweka yeye kuwa mkuu
ijapokuwa hakuwa mzaliwa wa
kwanza), 11 Hilkia wa pili, Tabalia
wa tatu na Zekaria wa nne. Wana
na jamaa za Hosa jumla yao
walikuwa watu kumi na watatu.

12 Hii migawanyo ya mabawabu,
kupitia wakuu wao, walikuwa na zamu za
kuhudumu hekaluni mwa BWANA kama
jamaa zao walivyokuwa nazo. 13 [b]Kura
zilipigwa kwa kila lango, kufuatana na
jamaa zao, wakubwa kwa wadogo.
14 [c]Kura ya Lango la Mashariki
ilimwangukia Shelemia.[d] Kisha wakapiga
kura kwa Zekaria mwanawe, aliyekuwa
mshauri mwenye hekima, nayo kura
ya Lango la Kaskazini ikamwangukia.
15 [e]Kura ya Lango la Kusini ikamwangukia
Obed-Edomu, nayo kura ya maghala
ikawaangukia wanawe. 16 [f]Kura za Lango
la Magharibi na Lango la Shalekethi kwenye
barabara ya juu zikawaangukia Shupimu
na Hosa.

Zamu za walinzi ziligawanywa kwa
usawa: 17 Kulikuwa na Walawi sita
kila siku upande wa mashariki, wanne
upande wa kaskazini, wanne upande wa
kusini, na wawili wawili kwa mara moja
kwenye ghala. 18 Kuhusu ukumbi kuelekea
magharibi, kulikuwa na wanne barabarani
na wawili kwenye ukumbi wenyewe.

19 [g]Hii ndiyo iliyokuwa migawanyo ya
mabawabu waliokuwa wazao wa Kora na
wa Merari.

*Watunza Hazina Na Maafisa Wengine*

20 [h]Katika Walawi, Ahiya alikuwa
mwangalizi wa hazina za nyumba ya
Mungu na mwangalizi wa hazina za vitu
vilivyowekwa wakfu.

21 [i]Wazao wa Ladani, waliokuwa
Wagershoni kupitia Ladani na waliokuwa
viongozi wa jamaa za Ladani Mgershoni,
walikuwa Yehieli, 22 wana wa Yehieli, wana
wa Zethamu na wa nduguye Yoeli. Wao
walikuwa waangalizi wa hazina za Hekalu
la BWANA.

23 [j]Kutoka kwa wana wa Amramu, wana
wa Ishari, wana wa Hebroni na wana wa
Uzieli:

24 [k]Shebueli, mzao wa Gershomu
mwana wa Mose, alikuwa afisa
mwangalizi wa hazina. 25 [l]Jamaa
zake kutoka kwa Eliezeri, wanawe
walikuwa: Rehabia, Yeshaya,
Yoramu, Zikri na Shelomithi.
26 [m]Shelomithi na jamaa zake
walikuwa waangalizi wa hazina
zote za vitu vile vilivyowekwa
wakfu na Mfalme Daudi, kwa
viongozi wa jamaa waliokuwa
majemadari wa maelfu na
majemadari wa mamia, na
kwa maafisa wengine wa jeshi.
27 [n]Baadhi ya nyara zilizotekwa
vitani waliziweka wakfu kwa
ajili ya ukarabati wa Hekalu la
BWANA. 28 [o]Kila kitu kilichokuwa
kimewekwa wakfu na Samweli
mwonaji, na Sauli mwana wa
Kishi, Abneri mwana wa Neri, na
Yoabu mwana wa Seruya, pamoja
na vitu vingine vyote vilivyokuwa

---

[a]**26:10** Kum 21:16-17; 1Nya 16:38; 5:1; Mwa 4:7; 49:3
[b]**26:13** 1Nya 24:5; 25:8; Mit 18:18; Yos 18:10; Yn 1:7; Mdo 1:26; 10:34; Gal 3:28; Kol 3:11
[c]**26:14** 1Nya 9:18-21
[d]14 Shelemia jina lingine ni Meshelemia.
[e]**26:15** 1Nya 13:13; 2Nya 25:24
[f]**26:16** 1Fal 10:5; 1Nya 24:31; Neh 12:24; 2Nya 9:4; 1Nya 25:8
[g]**26:19** Neh 7:1; Eze 44:11
[h]**26:20** 2Nya 24:5; 1Nya 28:12; 22:14-16; Kum 12:6; 1Fal 7:51; 14:26; 1Nya 9:26-29; Mal 3:10; 2Nya 31:11-12
[i]**26:21** 1Nya 6:17; 23:8; 29:8
[j]**26:23** Hes 3:27; Kut 6:18; 1Nya 23:12
[k]**26:24** 1Nya 23:16-18; 24:20
[l]**26:25** 1Nya 23:18; 24:22
[m]**26:26** 2Sam 8:11
[n]**26:27** Hes 31:50; Yos 6:19, 24; 1Nya 22:14-16; 2Nya 15:11, 18; 2Fal 12:14; 22:4-5; Neh 10:32
[o]**26:28** 1Sam 9:9

vimewekwa wakfu, vyote vilikuwa chini ya uangalizi wa Shelomithi na jamaa zake.

29 [a]Kutoka kwa wana wa Ishari:
Kenania na wanawe walipewa kazi nje ya Hekalu kama maafisa na waamuzi juu ya Israeli.

30 [b]Kutoka kwa wana wa Hebroni:
Hashabia na jamaa zake, watu 1,700 wenye uwezo, waliwajibika katika Israeli magharibi ya Yordani kwa ajili ya kazi zote za BWANA na utumishi wa mfalme.
31 [c]Kuhusu wana wa Hebroni, Yeria alikuwa mkuu wao kufuatana na orodha ya jamaa yao. Katika mwaka wa arobaini wa utawala wa Daudi uchunguzi ulifanyika katika kumbukumbu, nao watu wenye uwezo miongoni mwa wana wa Hebroni wakapatikana huko Yazeri katika Gileadi.
32 [d]Yeria alikuwa na jamaa ya watu 2,700 waliokuwa watu wenye uwezo na viongozi wa jamaa, naye Mfalme Daudi akawaweka kuangalia Wareubeni, Wagadi na nusu ya kabila Manase kuhusu kila jambo lililomhusu Mungu na shughuli za mfalme.

*Vikosi Vya Jeshi*

27 Hii ndiyo orodha ya Waisraeli: viongozi wa jamaa, majemadari wa maelfu, majemadari wa mamia na maafisa wao, waliomtumikia mfalme kwa lolote lililohusu vikosi vya jeshi vilivyokuwa zamu mwezi baada ya mwezi katika mwaka mzima. Kila kikosi kimoja kilikuwa na watu 24,000.

2 [e]Msimamizi wa kikosi cha kwanza kwa mwezi wa kwanza alikuwa Yashobeamu mwana wa Zabdieli. Kulikuwa na watu 24,000 katika kikosi chake.
3 [f]Yeye alikuwa mzao wa Peresi, na mkuu wa maafisa wote wa jeshi kwa mwezi wa kwanza.

4 [g]Msimamizi wa kikosi kwa mwezi wa pili alikuwa Dodai Mwahohi. Miklothi ndiye alikuwa kiongozi wa kikosi chake. Kikosi chake kilikuwa na watu 24,000.

5 [h]Jemadari wa kikosi cha tatu kwa mwezi wa tatu alikuwa Benaya mwana wa kuhani Yehoyada. Ndiye alikuwa mkuu wa kikosi chake kilichokuwa na watu 24,000.
6 [i]Huyu ndiye yule Benaya aliyekuwa shujaa miongoni mwa wale Thelathini na ndiye alikuwa juu yao hao Thelathini. Mwanawe Amizabadi ndiye alikuwa mkuu katika kikosi chake.

7 [j]Jemadari wa nne kwa mwezi wa nne alikuwa Asaheli nduguye Yoabu, mwanawe Zebadia ndiye aliingia mahali pake kwenye uongozi. Kikosi chake kilikuwa na watu 24,000.

8 Jemadari wa kikosi cha tano kwa mwezi wa tano alikuwa Shamhuthi Mwizrahi. Kikosi chake kilikuwa na watu 24,000.

9 [k]Jemadari wa kikosi cha sita kwa mwezi wa sita alikuwa Ira, mwana wa Ikeshi Mtekoa. Kikosi chake kilikuwa na watu 24,000.

10 Jemadari wa kikosi cha saba kwa mwezi wa saba alikuwa Helesi Mpeloni wa Waefraimu. Kikosi chake kilikuwa na watu 24,000.

11 [l]Jemadari wa nane kwa mwezi wa nane, alikuwa Sibekai Mhushathi wa Wazera. Kikosi chake kilikuwa na watu 24,000.

[a]**26:29** Kum 17:8-13; Neh 11:16; 2Nya 19:8-11; 1Nya 23:4
[b]**26:30** 1Nya 27:17
[c]**26:31** 1Nya 23:19; 2Sam 5:4; Isa 16:9; Yer 48:32; 1Fal 2:11; 1Nya 29:27; Yos 21:39
[d]**26:32** 2Nya 19:11
[e]**27:2** 2Sam 23:8; 1Nya 11:11
[f]**27:3** Mwa 38:29
[g]**27:4** 2Sam 23:9-20
[h]**27:5** 1Fal 4:5
[i]**27:6** 2Sam 23:20-23
[j]**27:7** 2Sam 2:18; 1Nya 11:26-28; 2Sam 23:24
[k]**27:9** 2Sam 23:26; 1Nya 11:28
[l]**27:11** 2Sam 21; 18; 1Nya 11:29

12 [a]Jemadari wa tisa kwa mwezi wa tisa alikuwa Abiezeri Mwanathothi wa Wabenyamini. Kikosi chake kilikuwa na watu 24,000.
13 [b]Jemadari wa kumi kwa mwezi wa kumi alikuwa Maharai Mnetofathi wa Wazera. Kikosi chake kilikuwa na watu 24,000.
14 [c]Jemadari wa kumi na moja kwa mwezi wa kumi na moja alikuwa Benaya Mpirathoni wa Waefraimu. Kikosi chake kilikuwa na watu 24,000.
15 [d]Jemadari wa kumi na mbili kwa mwezi wa kumi na mbili alikuwa Heldai Mnetofathi kutoka jamaa ya Othnieli. Kikosi chake kilikuwa na watu 24,000.

*Maafisa Wa Makabila*

16 Maafisa waliokuwa wanaoongoza makabila ya Israeli walikuwa:

Kwa Wareubeni: Eliezeri mwana wa Zikri;
kwa Wasimeoni: Shefatia mwana wa Maaka;
17 [e]kwa Walawi: Hashabia mwana wa Kemueli;
kwa Aroni: Sadoki;
18 [f]kwa Yuda: Elihu, nduguye Daudi;
kwa Waisakari: Omri mwana wa Mikaeli;
19 kwa Wazabuloni: Ishmaya mwana wa Obadia;
kwa Wanaftali: Yeremothi mwana wa Azrieli;
20 kwa Waefraimu: Hoshea mwana wa Azazia;
kwa nusu ya kabila la Manase: Yoeli mwana wa Pedaya;
21 kwa nusu nyingine ya kabila la Manase huko Gileadi: Ido mwana wa Zekaria;
kwa Wabenyamini: Yaasieli mwana wa Abneri;
22 kwa Wadani: Azareli mwana wa Yerohamu.

Hao ndio waliokuwa maafisa wa makabila ya Israeli.

23 [g]Daudi hakuwahesabu watu waliokuwa
chini ya miaka ishirini, kwa sababu BWANA
alikuwa ameahidi kuwafanya Israeli kuwa
wengi kama nyota za angani. 24 [h]Yoabu
mwana wa Seruya alianza kuwahesabu watu lakini hakumaliza. Kwa sababu ya kuwahesabu watu, hasira ya Mungu iliwaka juu ya Israeli, nayo hiyo hesabu yao haikuingizwa katika kitabu cha kumbukumbu za Mfalme Daudi.

*Wasimamizi Wa Mali Za Mfalme*

25 Azmawethi mwana wa Adieli ndiye alikuwa msimamizi wa hazina za mfalme.

Msimamizi wa hazina katika mashamba, miji, vijiji na kwenye ngome alikuwa Yonathani mwana wa Uzia.

26 Ezri mwana wa Kelubu alikuwa msimamizi wa wafanyakazi waliolima katika mashamba.

27 [i]Shimei Mramathi alikuwa msimamizi wa mashamba ya mizabibu.

Zabdi Mshifmi alikuwa msimamizi wa zabibu, utengenezaji na uhifadhi wa divai katika mapipa makubwa.

28 [j]Baal-Hanani Mgederi ndiye alikuwa mwangalizi wa mashamba ya mfalme ya mizeituni na mikuyu katika tambarare za vilima vya magharibi.

Yoashi alikuwa msimamizi wa ghala za mafuta ya zeituni.

29 Shitrai Msharoni alikuwa msimamizi wa makundi ya ng'ombe waliojilisha huko Sharoni.

Shafati mwana wa Adlai alikuwa msimamizi wa yale makundi ya ng'ombe yaliyokuwa makondeni.

---

[a]**27:12** 2Sam 23:27; 1Nya 11:30-31
[b]**27:13** 2Sam 23:28; 1Nya 11:36
[c]**27:14** 2Sam 23:30; 1Nya 11:31
[d]**27:15** 2Sam 23:29; Yos 15:17; Amu 3:9
[e]**27:17** 1Nya 26:30; 2Sam 8:17; 1Nya 12:28
[f]**27:18** 1Sam 16:6
[g]**27:23** 2Sam 24:1; 1Nya 21:2-5; Mwa 12:2; 15:5; Kut 32:13; Ebr 11:12
[h]**27:24** 2Sam 24:15; 1Nya 21:7
[i]**27:27** Wim 8:11
[j]**27:28** 1Fal 10:27; 2Nya 1:15

30 Obili Mwishmaeli alikuwa msimamizi
wa ngamia.
Yedeya Mmeronothi alikuwa msimamizi
wa punda.
31 [a]Yazizi Mhagri alikuwa msimamizi wa
makundi ya kondoo na mbuzi.
Hawa wote ndio waliokuwa maafisa
wasimamizi wa mali alizokuwa nazo
Mfalme Daudi.

32 [b]Yonathani mjomba wa Daudi alikuwa
mshauri, mtu mwenye ufahamu mkubwa
na mwandishi. Yehieli mwana wa Hakmoni
alikuwa akiwahudumia wana wa mfalme.
33 [c]Ahithofeli alikuwa mshauri wa
mfalme.
Hushai Mwariki alikuwa rafiki wa
mfalme. 34 [d]Baada ya Ahithofeli, Yehoyada
mwana wa Benaya aliingia mahali pake
kama mshauri wa mfalme pamoja na
Abiathari.
Yoabu alikuwa ndiye jemadari wa
majeshi ya mfalme.

*Maandalizi Ya Daudi Ya Kujenga Hekalu*

28 [e]Daudi akawaita maafisa wote wa Israeli
wakusanyike huko Yerusalemu: yaani,
maafisa walio juu ya makabila, majemadari
wa vikosi katika utumishi wa mfalme,
majemadari wa maelfu na majemadari wa
mamia, maafisa wanaosimamia mali zote na
mifugo ya mfalme na wanawe, wakiwemo
maafisa wa jumba la kifalme, mashujaa na
askari wote walio hodari.
2 [f]Mfalme Daudi akainuka na kusema:
"Nisikilizeni ndugu zangu nanyi watu
wangu. Nilikuwa na nia ya kujenga nyumba
ili iwe mahali pa kukaa Sanduku la Agano
la BWANA kwa ajili ya kuwa mahali pa
kuwekea miguu ya Mungu wetu, nami
nikafanya maandalizi ya kuijenga. 3 [g]Lakini
Mungu akaniambia, 'Wewe hutajenga
nyumba kwa Jina langu, kwa sababu wewe
umepigana vita na umemwaga damu.'
4 [h]"Hata hivyo, BWANA, Mungu wa
Israeli, alinichagua mimi kutoka jamaa
yangu yote niwe mfalme juu ya Israeli
milele. Alimchagua Yuda kuwa kiongozi
na kutoka nyumba ya Yuda akaichagua
jamaa yangu na kutoka wana wa baba
yangu ikampendeza kunifanya niwe
mfalme juu ya Israeli yote. 5 [i]Miongoni
mwa wanangu wote, naye BWANA amenipa
wengi, amemchagua Solomoni mwanangu
ili kukikalia kiti cha enzi cha ufalme wa
BWANA juu ya Israeli. 6 [j]Aliniambia,
'Solomoni mwanao ndiye atakayejenga
nyumba yangu na nyua zangu, kwa maana
nimemchagua yeye kuwa mwanangu, nami
nitakuwa baba yake. 7 [k]Nitaufanya imara
ufalme wake milele kama akiendelea
kuzishika amri zangu na sheria zangu, kama
afanyavyo hivi leo.'
8 [l]"Hivyo basi ninawaagiza mbele za
Israeli yote na kusanyiko hili la BWANA
naye Mungu wetu akiwa anasikia: Kuweni
na bidii kuzifuata amri za BWANA Mungu
wenu, ili mpate kumiliki nchi hii nzuri na
kuwaachia wana wenu kuwa urithi milele.
9 [m]"Nawe Solomoni mwanangu, mjue
Mungu wa baba yako, ukamtumikie
kwa kujitoa kwa moyo wote na kwa
nia ya kumkubali, kwa maana BWANA
huuchunguza kila moyo na kujua
kila kusudi la kila fikira. Ukimtafuta,
ataonekana kwako; bali kama ukimwacha,

---

[a]**27:31** 1Nya 5:10
[b]**27:32** 2Sam 21:21
[c]**27:33** 2Sam 15:12, 37
[d]**27:34** 1Sam 22:20; 2Sam 2:13; 1Nya 11:6
[e]**28:1** 1Nya 11:10; 29:6; Kut 18:25; 1Nya 27:16; Yos 23:2; 24:1; 1Nya 23:2; Kum 1:15
[f]**28:2** 1Sam 10:7; 1Nya 17:2; Za 132:7; Isa 60:13; Ebr 2:11; Kum 17:20; 1Nya 11:1-3; Za 22:22; 2Sam 7:2; 1Fal 8:17; 2Nya 6:7-8
[g]**28:3** 2Sam 7:5; 1Nya 22:8; 1Fal 5:3; 1Nya 17:4
[h]**28:4** 1Nya 17:23-27; 2Nya 6:6; 1Sam 16:1-13; Mwa 49:10; Hes 24:17-19
[i]**28:5** 1Nya 3:1; 2Sam 12:24; 1Nya 22:9; 14:4-7
[j]**28:6** 2Sam 7:13; 1Nya 22:9-10
[k]**28:7** 1Nya 22:13; 1Fal 9:4; 11:11
[l]**28:8** Kum 6:1; 4:1; 17:14-20
[m]**28:9** 1Nya 29:19; 2Nya 6:30; Za 40:16; Yer 29:13; Kum 4:31; Yos 24:20; Za 9:10; Yer 9:24; Yn 17:3; 2Fal 20:3; Za 101:2; 1Sam 16:7; 1Fal 8:39; 1Nya 29:17; Ufu 2:23; 2Nya 15:2; Mt 7:7; Yak 4:8-10

yeye atakukataa milele. 10 [a]Angalia basi,
kwa maana Bwana amekuchagua wewe
ili ujenge Hekalu kuwa mahali patakatifu.
Uwe hodari ukafanye kazi hiyo.”
11 [b]Ndipo Daudi akampa Solomoni
mwanawe kielelezo kwa ajili ya ukumbi wa
Hekalu, nyumba zake, vyumba vyake vya
hazina, ghorofa zake, vyumba vyake vya
ndani na mahali pa kufanyia upatanisho.
12 [c]Akampa vielelezo vya yote Roho alikuwa
ameviweka moyoni mwake kwa ajili ya
kumbi za Hekalu la Bwana na vyumba
vyote vilivyolizunguka, kwa ajili ya hazina
za Hekalu la Mungu na kwa hazina za vitu
vilivyowekwa wakfu. 13 Mfalme pia akampa
Solomoni maelekezo kwa ajili ya migawanyo
ya huduma za makuhani na Walawi, pia
kwa ajili ya kazi zote za huduma katika
Hekalu la Bwana. Akampa pia maelezo
kuhusu vifaa vyote vya kutumika katika
huduma ya Hekalu. 14 Akamwagizia uzito
wa dhahabu kwa ajili ya vitu vyote vya
dhahabu vya kutumika katika huduma
mbalimbali, uzito wa fedha kwa ajili ya
vitu vyote vya fedha vya kutumika katika
huduma mbalimbali. 15 [d]Uzito wa dhahabu
kwa ajili ya vinara vya dhahabu na taa zake,
kukiwa na uzito kwa ajili ya kila kinara na
taa zake, pamoja na uzito wa fedha kwa
ajili ya kila kinara cha fedha na taa zake,
kulingana na matumizi ya kila kinara;
16 [e]uzito wa dhahabu kwa ajili ya meza ya
mikate iliyowekwa wakfu, uzito wa fedha
kwa ajili ya meza ya fedha; 17 [f]uzito wa
dhahabu safi kwa ajili ya nyuma, mabakuli
ya kunyunyizia na vikombe, masinia; uzito
wa dhahabu kwa ajili ya kila bakuli la
dhahabu; uzito wa fedha kwa ajili ya kila
bakuli la fedha; 18 [g]na uzito wa dhahabu
safi kwa ajili ya madhabahu ya kufukizia
uvumba. Pia alimpa kielelezo kwa ajili ya
gari, yaani, wale makerubi wa dhahabu
waliokunjua mbawa zao na kuweka kivuli
juu ya Sanduku la Agano la Bwana.
19 [h]Daudi akasema, “Hii yote, ninayo kwa
maandishi kutoka mkononi mwa Bwana
ulio juu yangu, naye amenipa ufahamu kwa
ajili ya habari zote za kielelezo hiki.”
20 [i]Daudi pia akamwambia Solomoni
mwanawe, “Uwe hodari na moyo
mkuu, ukafanye kazi hii. Usiogope wala
usifadhaike, kwa maana Bwana aliye
Mungu, Mungu wangu yu pamoja nawe.
Hatakuacha wala hatakupungukia mpaka
kazi hii yote kwa ajili ya utumishi wa Hekalu
la Bwana itakapokamilika. 21 [j]Migawanyo
ya makuhani na Walawi iko tayari kwa
ajili ya kazi yote katika Hekalu la Mungu,
naye kila mtu mwenye moyo wa kupenda
mwenye ustadi katika aina yoyote ya ufundi
atakusaidia katika kazi yote. Maafisa na
watu wote watatii kila agizo lako.”

*Matoleo Kwa Ajili Ya Ujenzi Wa Hekalu*

29 [k]Ndipo Mfalme Daudi akaliambia
kusanyiko lote: “Mwanangu Solomoni,
yeye ambaye Mungu amemchagua, ni
kijana mdogo na asiye na uzoefu. Kazi
hii ni kubwa, kwa sababu Hekalu hili la
fahari si kwa ajili ya mwanadamu bali ni
kwa ajili ya Bwana. 2 [l]Kwa uwezo wangu
wote nimetenga mali kwa ajili ya Hekalu
la Mungu wangu: dhahabu kwa kazi za
dhahabu, fedha kwa ajili ya fedha, shaba
kwa kazi za shaba, chuma kwa kazi za
chuma na miti kwa kazi za miti, vivyo hivyo
vito vya shohamu kwa ajili ya kutia kwenye
vijalizo, almasi, mawe ya rangi mbalimbali,
aina zote za vito vya thamani na marmar;
yote haya kwa wingi mno. 3 [m]Zaidi ya hayo,
kwa kujitolea kwangu kwa ajili ya Hekalu
la Mungu wangu, sasa ninatoa hazina zangu

[a]**28:10** 1Nya 22:16; Mit 4:23
[b]**28:11** Kut 25:9; Ebr 8:9; 1Fal 6:2
[c]**28:12** 1Nya 12:18; 26:12-20
[d]**28:15** Kut 25:31
[e]**28:16** Kut 25:23; 1Fal 7:48; 2Nya 4:8
[f]**28:17** Kut 27:3
[g]**28:18** Kut 30:1-10; 25:22; Eze 10:2; Za 68:17; 1Fal 6:23; Za 18:10
[h]**28:19** 1Fal 6:38; Kut 25:9; 25:40; 26:30
[i]**28:20** 2Nya 29:11; Hag 2:4; Kum 4:31; Yos 24:20; 1Fal 6:14; Ebr 13:5; Kum 31:7; Yos 1:5-7; 1Nya 22:13; 1Kor 16:13
[j]**28:21** 1Nya 25:1; Kut 35:25–36:5
[k]**29:1** 1Fal 3:7; 2Nya 13:7; Mit 4:3; 1Nya 22:5
[l]**29:2** Ezr 6:5; Ufu 21:18; Hag 2:8; Isa 54:11; 1Nya 22:2-5; Kut 28:9
[m]**29:3** 2Nya 24:10; Za 28:9; 2Nya 35:8; Za 26:8; 27:4; Mit 3:9

mwenyewe za dhahabu na fedha kwa ajili
ya Hekalu la Mungu wangu, zaidi ya mali
niliyotoa kwa ajili ya Hekalu hili takatifu:
4 [a]talanta 3,000[b] za dhahabu (dhahabu
ya Ofiri) na talanta 7,000[c] za fedha safi
iliyosafishwa, kwa ajili ya kufunika kuta za
Hekalu, 5 kwa kazi ya dhahabu na kazi ya
fedha na kwa kazi yote itakayofanywa na
mafundi. Basi, ni nani anayependa kujitoa
kwa BWANA leo?"

6 [d]Ndipo viongozi wa jamaa, maafisa wa
kabila za Israeli, majemadari wa maelfu na
majemadari wa mamia, pamoja na maafisa
waliokuwa wasimamizi wa kazi za mfalme
wakatoa kwa hiari yao.

7 Wakatoa kwa ajili ya kazi ya Hekalu la
Mungu talanta 5,000[e] na darkoni 10,000[f] za
dhahabu, talanta 10,000[g] za fedha, talanta
18,000[h] za shaba na talanta 100,000[i] za
chuma. 8 [j]Kila mmoja aliyekuwa na vito
vya thamani akavitoa katika hazina ya
Hekalu la BWANA chini ya uangalizi wa
Yehieli Mgershoni. 9 [k]Watu wakafurahi kwa
sababu ya itikio la hiari la viongozi wao,
kwa kuwa walikuwa wametoa kwa hiari
na kwa moyo wote kwa BWANA. Mfalme
Daudi pia akafurahi sana.

*Maombi Ya Daudi*

10 [l]Daudi akamhimidi BWANA mbele ya
kusanyiko lote, akisema:

"Uhimidiwe wewe, Ee BWANA,
Mungu wa Israeli baba yetu,
tangu milele hata milele.
11 [m]Ukuu na uweza, ni vyako, Ee
BWANA,
na utukufu na enzi na uzuri,
kwa kuwa kila kilichoko mbinguni
na duniani
ni chako wewe.
Ee BWANA, ufalme ni wako;
umetukuzwa kuwa mkuu juu ya
yote.
12 [n]Utajiri na heshima vyatoka kwako;
wewe ndiwe utawalaye vitu vyote.
Mikononi mwako kuna nguvu na
uweza
ili kuinua na kuwapa wote nguvu,
13 Sasa, Mungu wetu, tunakushukuru
na kulisifu Jina lako tukufu.

14 "Lakini mimi ni nani, nao watu wangu
ni nani, hata tuweze kukutolea kwa ukarimu
namna hii? Vitu vyote vyatoka kwako, nasi
tumekutolea tu vile vitokavyo mkononi
mwako. 15 [o]Sisi ni wageni na wapitaji
machoni pako, kama walivyokuwa baba
zetu wote. Siku zetu duniani ni kama kivuli,
bila tumaini. 16 Ee BWANA Mungu wetu,
kwa wingi wote huu ambao tumekutolea
kwa kujenga Hekalu kwa ajili ya Jina lako
Takatifu, vimetoka mkononi mwako, navyo
vyote ni mali yako. 17 [p]Ninajua, Mungu
wangu, kwamba wewe huujaribu moyo
na unapendezwa na unyofu. Vitu hivi
vyote nimetoa kwa hiari na kwa moyo
mnyofu. Nami sasa nimeona kwa furaha
jinsi watu wako walioko hapa kwa hiari
yao walivyokutolea wewe. 18 [q]Ee BWANA,
Mungu wa baba zetu Abrahamu, Isaki na

[a]**29:4** Mwa 10:29; 1Nya 22:14; Ay 22:24; 1Fal 9:28; 2Nya 8:18
[b]4 Talanta 3,000 za dhahabu sawa na tani 110.
[c]4 Talanta 7,000 za fedha ni sawa na tani 260.
[d]**29:6** 1Nya 28:1; Kut 36:2; Ezr 7:15
[e]7 Talanta 5,000 za dhahabu ni sawa na tani 190.
[f]7 Darkoni 10,000 za dhahabu ni sawa na kilo 84.
[g]7 Talanta 10,000 za fedha ni sawa na tani 375.
[h]7 Talanta 18,000 za shaba ni sawa na tani 675.
[i]7 Talanta 100,000 za chuma ni sawa na tani 3,750.
[j]**29:8** Kut 35:27; 1Nya 26:21
[k]**29:9** 1Fal 8:61; 2Kor 9:7
[l]**29:10** 1Fal 8:15-16; 2Nya 6:4; Za 72:18; Eze 3:12
[m]**29:11** Za 24:8; 89:11; Mt 6:13; Ufu 5:12-13; Dan 4:34-35; 1Tim 1:17
[n]**29:12** Ezr 7:27; Mhu 5:19; 2Nya 20:6; Rum 11:36; Kum 8:18; 1Sam 2:7-8; Za 75:6; Mit 10:22; Yak 1:17
[o]**29:15** Mwa 47:9; 23:4; Ebr 11:13; Mhu 6:12; Za 102:11; Ay 14:2; Za 39:12; 1Pet 2:11; Za 90:9; 144:4
[p]**29:17** Mit 17:3; Yer 11:20; Za 15:1-5; Mit 11:20; Ebr 4:13; Kum 8:2; 1Sam 16:7; 1Nya 28:9; Za 7:9; Yer 17:10; Mit 16:2
[q]**29:18** Za 10:17; Yer 10:23

Israeli, weka shauku hii ndani ya mioyo ya
watu wako daima na uifanye mioyo yao
iwe na uaminifu kwako. 19 [a]Nawe umpe
mwanangu Solomoni kujitolea kwako kwa
moyo wote ili kuzishika amri zako, masharti
yako, maagizo yako na kufanya kila kitu ili
kujenga Hekalu hili la fahari ambalo kwa
ajili yake nimetoa."

20 Ndipo Daudi akaliambia kusanyiko
lote, "Mhimidini BWANA Mungu wenu."
Hivyo wote wakamhimidi BWANA, Mungu
wa baba zao. Wakasujudu na kuanguka
kifudifudi mbele za BWANA na mfalme.

*Solomoni Akubalika Kuwa Mfalme*

21 Siku ya pili yake wakamtolea BWANA
dhabihu na sadaka za kuteketezwa: mafahali
1,000, kondoo dume 1,000 na wana-kondoo
dume 1,000, pamoja na sadaka za kinywaji
na sadaka nyingine nyingi sana kwa ajili ya
Israeli. 22 [b]Wakala na kunywa kwa furaha
kubwa mbele za BWANA siku ile.

Wakamtawaza Solomoni mwana wa
Daudi mara ya pili kuwa mfalme, wakamtia
mafuta kwa ajili ya BWANA ili awe mfalme
na Sadoki kuwa kuhani. 23 [c]Solomoni
akaketi kwenye kiti cha enzi cha BWANA
kuwa mfalme mahali pa Daudi baba yake.
Akafanikiwa sana na Israeli wote wakamtii.
24 [d]Maafisa wote na mashujaa, pamoja na
wana wote wa Daudi, wakaahidi kumtii
Mfalme Solomoni.

25 [e]BWANA akamtukuza sana Solomoni
mbele ya Israeli wote na kumvika fahari
ya kifalme ambayo hakuna mfalme yeyote
wa Israeli kabla yake aliwahi kuwa nayo.

*Muhtasari Wa Utawala Wa Daudi*

26 [f]Daudi mwana wa Yese alikuwa
mfalme wa Israeli yote. 27 [g]Alitawala
Israeli kwa miaka arobaini: huko Hebroni
alitawala miaka saba, na katika Yerusalemu
akatawala miaka thelathini na mitatu.

28 [h]Daudi akafa akiwa mzee mwenye umri
mwema, akiwa ameshiba siku, utajiri na
heshima. Naye Solomoni mwanawe akawa
mfalme baada yake.

29 [i]Kuhusu matukio ya utawala wa Mfalme
Daudi, kuanzia mwanzo hadi mwisho,
yameandikwa katika kumbukumbu za
mwonaji Samweli, na kumbukumbu za
nabii Nathani na kumbukumbu za mwonaji
Gadi, 30 [j]pamoja na habari zote za utawala
wake, nguvu zake na matukio yaliyompata
yeye, na Israeli, na falme za nchi nyingine
zote.

---

[a]**29:19** 1Fal 8:61; Isa 38:3; 1Nya 22:14; Za 72:1
[b]**29:22** 1Nya 12:40; 1Sam 2:35; 1Fal 1:33-39
[c]**29:23** 1Fal 2:12; 1Nya 17:14
[d]**29:24** Mwa 24:2; 47:29; Eze 17:18; 2Nya 30:8
[e]**29:25** 1Fal 10:7; 3:13; Mhu 2:9; 2Nya 1:12; Dan 5:18-19; Ebr 2:9
[f]**29:26** 1Nya 18:14
[g]**29:27** 2Sam 5:4-5; 1Fal 2:11
[h]**29:28** Mwa 15:15; Mdo 13:36; 1Nya 23:1; Mwa 25:8; Hes 23:10; Ay 5:26
[i]**29:29** 1Sam 9:9; 22:5; 2Sam 7:2; Ay 5:26
[j]**29:30** Dan 2:21

# 2 MAMBO YA NYAKATI

*Solomoni Aomba Hekima*

**(1 Wafalme 3:1-15)**

1 [a]Solomoni mwana wa Daudi alijiimarisha
kwenye milango yote! Katika ufalme
wake, kwa kuwa BWANA Mungu wake
alikuwa pamoja naye, naye akamfanya
mkuu mno.
2 [b]Ndipo Solomoni akasema na
Israeli wote, majemadari wa maelfu na
majemadari wa mamia, waamuzi na
viongozi wote katika Israeli, pamoja na
wakuu wa jamaa. 3 [c]Naye Solomoni na
kusanyiko lote wakakwea mpaka mahali
pa juu pa kuabudia huko Gibeoni, kwa
kuwa huko ndiko Hema la Kukutania la
Mungu lilipokuwa, ambalo Mose mtumishi
wa BWANA alikuwa amelitengeneza
huko jangwani. 4 [d]Basi Daudi alikuwa
amelipandisha Sanduku la Mungu kutoka
Kiriath-Yearimu mpaka mahali alipokuwa
amepatengeneza kwa ajili yake, kwa sababu
alikuwa amesimamisha hema kwa ajili ya
hilo Sanduku huko Yerusalemu. 5 [e]Lakini
yale madhabahu ya shaba ambayo Bezaleli
mwana wa Uri, mwana wa Huri, alikuwa
ametengeneza yalikuwa huko Gibeoni
mbele ya Maskani ya BWANA Mungu, hivyo
Solomoni na kusanyiko lote walimtafuta
Mungu huko. 6 [f]Solomoni akapanda huko
yalikokuwa madhabahu ya shaba mbele za
BWANA katika Hema la Kukutania, na kutoa
dhabihu 1,000 za sadaka za kuteketezwa
juu yake.
7 [g]Usiku ule Mungu akamtokea Solomoni
na kumwambia, “Omba lolote utakalo
nikupe.”
8 [h]Solomoni akamjibu Mungu,
“Umemwonyesha baba yangu Daudi fadhili
nyingi, nawe umeniweka niwe mfalme
mahali pake. 9 [i]Sasa, BWANA Mungu, ahadi
yako kwa baba yangu Daudi na ithibitike,
kwa kuwa umenifanya mimi mfalme juu ya
watu ambao ni wengi kama mavumbi ya
nchi. 10 [j]Nakuomba unipe mimi hekima na
maarifa, ili niweze kuongoza watu hawa,
kwa kuwa ni nani awezaye kutawala hawa
watu wako walio wengi hivi?”
11 [k]Mungu akamwambia Solomoni, “Kwa
kuwa jambo hili ndilo shauku ya moyo wako
na hukuomba mali, utajiri au heshima, wala
kifo kwa ajili ya adui zako, nawe kwa kuwa
hukuomba maisha marefu, bali umeomba
hekima na maarifa ili kuongoza watu
wangu ambao nimekufanya uwe mfalme
juu yao, 12 [l]kwa hiyo utapewa hekima na
maarifa. Tena nitakupa pia mali, utajiri
na heshima, ambavyo hakuna mfalme
yeyote aliyekuwepo kabla yako amewahi
kuwa navyo, na hakuna yeyote baada yako
atakayekuwa navyo.”

*Fahari Ya Solomoni*

**(1 Wafalme 10:26-29)**

13 Ndipo Solomoni akaenda mpaka
Yerusalemu kutoka mahali pa juu pa
kuabudia huko Gibeoni, kutoka mbele ya
Hema la Kukutania. Naye akatawala Israeli.
14 [m]Solomoni akakusanya magari ya vita
na farasi. Alikuwa na magari 1,400 na farasi
12,000, ambayo aliyaweka katika miji
ya magari na mengine akawa nayo huko
Yerusalemu. 15 [n]Mfalme akafanya fedha

[a]**1:1** 1Fal 2:26; 2Nya 12:1; Mwa 39:2; Hes 14:43; 1Nya 29:25; Mwa 21:22; 1Nya 17:8; Mt 28:20
[b]**1:2** 1Nya 28:1; 2Nya 29:20; 30:2
[c]**1:3** Law 17:4; Kut 36:8; 40:18; 1Fal 3:4
[d]**1:4** 2Sam 6:2, 17; 1Nya 15:25
[e]**1:5** Kut 38:2; 31:2; 1Nya 13:3
[f]**1:6** 1Fal 3:4
[g]**1:7** 2Nya 7:12; Isa 58:9; 1Fal 3:5; Mit 3:5
[h]**1:8** 1Nya 23:1; 28:5
[i]**1:9** 2Sam 7:25; 1Fal 8:25; Mwa 12:2
[j]**1:10** Hes 27:17; Mit 8:15-16; Kum 31:2; 1Fal 3:9; Za 119:34; Mit 3:13; Yak 1:5
[k]**1:11** Kum 17:17; 1Sam 16:7; 1Fal 3:11; 8:18
[l]**1:12** 1Nya 29:12-25; Neh 13:26; Efe 3:20; 2Nya 9:22; Za 34:9-10; Mt 6:33; Mhu 2:9
[m]**1:14** 1Sam 8:11; 1Fal 9:19; 4:26
[n]**1:15** 1Fal 9:28; Isa 60:5; Ay 22:24; 1Fal 10:27

na dhahabu kuwa vitu vya kawaida kama
mawe huko Yerusalemu, mierezi akaifanya
kuwa mingi kama mikuyu vilimani. 16 Farasi
wa Solomoni waliletwa kutoka Misri na
kutoka Kue.[a] Wafanyabiashara wa mfalme
waliwanunua kutoka Kue. 17 [b]Waliagiza
magari kutoka Misri kwa bei ya shekeli
600[c] za fedha, na farasi kwa shekeli 150.[d]
Pia waliwauza nje kwa wafalme wote wa
Wahiti na wa Waaramu.

*Maandalizi Ya Kujenga Hekalu*

**(1 Wafalme 5:1-18)**

2 [e]Solomoni akatoa amri kujenga Hekalu
kwa ajili ya Jina la BWANA na jumba
la kifalme kwa ajili yake mwenyewe.
2 [f]Solomoni akaandika watu 70,000 kuwa
wachukuzi wa mizigo, na watu 80,000
kuwa wachonga mawe vilimani, na watu
3,600 kuwa wasimamizi wao.
3 [g]Solomoni akapeleka ujumbe huu kwa
Mfalme Hiramu wa Tiro:

"Unitumie magogo ya mierezi kama
ulivyomfanyia baba yangu Daudi
wakati ulipompelekea mierezi ya
kujenga jumba lake la kifalme la kuishi.
4 [h]Sasa ninakaribia kujenga Hekalu kwa
ajili ya Jina la BWANA Mungu wangu
na kuliweka wakfu kwake kwa ajili
ya kufukizia uvumba wenye harufu
nzuri mbele zake, mahali pa kuweka
mikate ya Wonyesho kwa kufuata
utaratibu na kwa ajili ya mahali pa
kutolea sadaka za kuteketezwa kila
siku asubuhi na jioni, siku za Sabato na
Mwezi Mwandamo pia katika sikukuu
zilizoamriwa za BWANA Mungu wetu.
Hili ni agizo la kudumu kwa ajili ya
Waisraeli.
5 [i]"Hekalu nitakalolijenga litakuwa
kubwa, kwa sababu Mungu wetu ni
mkuu kuliko miungu mingine yote.
6 [j]Lakini ni nani awezaye kumjengea
Hekalu, maadamu mbingu, hata
mbingu zilizo juu sana, haziwezi
kumtosha? Mimi ni nani basi hata
nimjengee Hekalu, isipokuwa liwe
tu mahali pa kutolea dhabihu za
kuteketezwa mbele zake?
7 [k]"Hivyo basi nitumie mtu mwenye
ustadi wa kufanya kazi ya kutengeneza
dhahabu na fedha, shaba na chuma,
nyuzi za rangi ya zambarau, nyekundu
na buluu, mwenye uzoefu wa kutia
nakshi, ili afanye kazi Yuda na
Yerusalemu pamoja na mafundi wangu
wenye ustadi, ambao baba yangu
Daudi aliwaweka.
8 [l]"Pia nitumie magogo ya mierezi,
miberoshi na misandali kutoka
Lebanoni kwa maana najua kwamba
watu wako wanao ujuzi wa kupasua
mbao huko. Watu wangu watafanya
kazi pamoja na watu wako 9 ili
wanipatie mbao kwa wingi kwa sababu
Hekalu nitakalojenga lazima liwe
kubwa na zuri kabisa. 10 [m]Nitawapa
watumishi wako, yaani, maseremala
wakatao mbao, kori 20,000[n] za unga
wa ngano, kori 20,000 za shayiri, bathi
20,000[o] za mvinyo, na bathi 20,000 za
mafuta ya zeituni."

11 [p]Ndipo Hiramu mfalme wa Tiro
akamjibu Solomoni kwa barua:

"Kwa sababu BWANA anawapenda
watu wake, amekufanya wewe kuwa
mfalme wao."

[a]16 Yaani Kilikia.
[b]**1:17** Wim 1:9
[c]17 Shekeli 600 za fedha ni sawa na kilo 7.
[d]17 Shekeli 150 ni sawa na kilo 1.7.
[e]**2:1** Kum 12:5; 1Fal 5:5; Mhu 2:14
[f]**2:2** 2Nya 10:4; 1Fal 5:15
[g]**2:3** 2Sam 5:11; 1Nya 14:1
[h]**2:4** Kut 12:5; 25:30; Law 24:8; Kut 29:42; Hes 28:10; Kut 30:7; Mt 12:4
[i]**2:5** 1Nya 22:5; 16:25; Za 135:5; Kut 15:11; Za 86:8-9; Yer 10:6
[j]**2:6** 1Fal 8:27; Yer 23:24; 2Nya 6:28; Kut 3:11; Isa 66:1
[k]**2:7** Kut 35:31; 1Nya 22:16
[l]**2:8** 1Fal 5:6; 19:11
[m]**2:10** 1Fal 5:11; Ezr 3:7
[n]10 Kori 20,000 za ngano ni sawa na lita 4,400.
[o]10 Bathi 20,000 za mvinyo au mafuta ni sawa na lita 440,000.
[p]**2:11** 1Fal 10:9; 2Nya 9:8; Kum 33:3

12 [a]Naye Hiramu akaongeza kusema:

"Ahimidiwe BWANA, Mungu wa
Israeli aliyezifanya mbingu na nchi!
Amempa Mfalme Daudi mwana
mwenye hekima, aliyejaliwa maarifa
na ufahamu, ambaye atajenga Hekalu
kwa ajili ya BWANA, na jumba la
kifalme kwa ajili yake mwenyewe.
13 [b]"Mimi nitamtuma kwako Huramu-
Abi, mtu mwenye ustadi mwingi,
14 [c]ambaye mama yake alitoka Dani
na baba yake alitoka Tiro. Yeye ni
stadi wa kutengeneza vitu, kufanya
kazi zote za dhahabu, fedha, shaba,
chuma, mawe na mbao pamoja na
kufuma. Ni stadi katika kutia rangi ya
zambarau, buluu, nyekundu na nguo
za kitani safi. Yeye ana ujuzi katika
aina zote za kutia nakshi na anaweza
kufuatiliza mchoro wowote wa kazi
anayopewa. Atafanya kazi na mafundi
wako na wale wa bwana wangu, Daudi
baba yako.
15 "Sasa basi bwana wangu na
awapelekee watumishi wake ngano,
shayiri, mafuta ya zeituni na mvinyo
kama alivyoahidi, 16 [d]nasi tutakata
magogo yote yale unayohitaji kutoka
Lebanoni nasi tutayafunga pamoja na
kuyaweka yaelee baharini mpaka Yafa.
Kisha utaweza kuyachukua mpaka
Yerusalemu."

17 [e]Ndipo Solomoni akaamuru ifanyike
hesabu ya wageni wote waliokuwa katika
Israeli, baada ya ile hesabu iliyofanywa
na Daudi; wakapatikana watu 153,600.
18 Akawaweka watu 70,000 miongoni mwao
kuwa wachukuzi wa mizigo, na 80,000
kuwa wachonga mawe vilimani, na 3,600
wakiwa wasimamizi juu yao ili wawahimize
watu kufanya kazi.

*Solomoni Ajenga Hekalu*

**(1 Wafalme 6:1-38; 7:15-22)**

3 [f]Ndipo Solomoni akaanza kujenga
Hekalu la BWANA katika Yerusalemu
juu ya Mlima Moria, pale ambapo BWANA
alikuwa amemtokea Daudi baba yake.
Ilikuwa katika kiwanja cha kupuria cha
Arauna,[g] Myebusi, mahali palipotolewa
na Daudi. 2 [h]Alianza kujenga siku ya pili
ya mwezi wa pili katika mwaka wa nne
wa utawala wake.
3 [i]Msingi aliouweka Solomoni kwa ajili ya
kulijenga Hekalu la Mungu ulikuwa urefu
wa dhiraa sitini[j] na upana dhiraa ishirini.[k]
4 [l]Ukumbi wa mbele wa Hekalu ulikuwa
na urefu wa dhiraa ishirini, yaani, kuanzia
upande mmoja hadi upande mwingine wa
upana wa nyumba hiyo na kimo chake
dhiraa thelathini.[m]
Akaufunika ndani kwa dhahabu safi.
5 [n]Akaufunika ukumbi mkuu kwa mbao
za miberoshi na kufunikwa kwa dhahabu
safi na kuupamba kwa miti ya mitende na
kuifanyizia kwa minyororo. 6 Alilipamba
Hekalu kwa vito vya thamani. Hiyo
dhahabu aliyotumia ilikuwa dhahabu ya
Parvaimu. 7 [o]Akazifunika boriti za dari,
miimo na vizingiti vya milango, kuta na
milango ya Hekalu kwa dhahabu, naye
akatia nakshi ya makerubi kwenye kuta.
8 [p]Akajenga Patakatifu pa Patakatifu, urefu
na upana wake ulikuwa dhiraa ishirini,
sawasawa na upana wa Hekalu. Alifunika
ndani kwa talanta 120[q] za dhahabu safi.
9 Misumari ya dhahabu ilikuwa na uzito wa

[a]**2:12** Neh 9:6; Mdo 4:24; Za 146:6; 1Fal 5:7; Za 33:6; 102:25; Ufu 10:6
[b]**2:13** 1Fal 7:13
[c]**2:14** Kut 31:6; 35:31-35; 1Fal 7:13
[d]**2:16** Yos 19:46; Mdo 9:36; Yon 1:3; 1Fal 5:8
[e]**2:17** 1Nya 22:2; 2Sam 24:2; 2Nya 8:7-8; 1Fal 5:1

[f]**3:1** Mdo 7:47; Mwa 28:17; 2Sam 24:18; Yn 2:19-21; 1Fal 6:1; 1Nya 29:19; 1Kor 6:19; Mwa 22:2
[g]1 Pia anaitwa Ornani kwa Kiebrania.
[h]**3:2** Ezr 5:11
[i]**3:3** Eze 41:2; 1Fal 6:2-3
[j]3 Dhiraa 60 ni sawa na mita 27.
[k]3 Dhiraa 20 ni sawa na mita 9.
[l]**3:4** 1Fal 6:3
[m]4 Dhiraa 30 ni sawa na mita 13.5.
[n]**3:5** Eze 40:16; 1Fal 6:17
[o]**3:7** 1Fal 6:29-35; Eze 41:18
[p]**3:8** Kut 26:32-33
[q]8 Talanta 120 za dhahabu ni sawa na tani 23.

shekeli hamsini.[a] Alivifunika pia vyumba
vya juu kwa dhahabu.
10 [b]Katika sehemu ya Patakatifu pa
Patakatifu akafanyiza jozi moja ya makerubi
ya kuchongwa na kuyafunika kwa dhahabu.
11 Urefu wa mabawa ya hao makerubi
ulikuwa jumla ya dhiraa ishirini. Bawa moja
la kerubi wa kwanza lilikuwa na urefu wa
dhiraa tano,[c] nalo liligusa ukuta wa Hekalu,
bawa lake lingine, lilikuwa pia na urefu wa
dhiraa tano, ambalo liligusa bawa la kerubi
lingine. 12 Vivyo hivyo bawa moja la kerubi
wa pili lilikuwa na urefu wa dhiraa tano na
liligusa ukuta mwingine wa pili wa Hekalu
na bawa lake lingine, lilikuwa pia na urefu
wa dhiraa tano nalo liligusa bawa la kerubi
wa kwanza. 13 Mabawa ya makerubi hawa
yalitanda dhiraa ishirini. Walisimama kwa
miguu yao, nyuso zao zikielekea ukumbi
mkubwa.
14 [d]Akatengeneza pazia la nyuzi za rangi
ya buluu, zambarau na nyekundu, na za
kitani safi, na kutarizi makerubi juu yake.
15 [e]Mbele ya Hekalu Solomoni
akatengeneza nguzo mbili, ambazo kwa
pamoja zilikuwa na dhiraa thelathini
na tano kwenda juu kwake, na urefu wa
kila moja ilikuwa na taji juu yake yenye
dhiraa tano. 16 [f]Akatengeneza minyororo
iliyosokotwa, na kuiweka juu ya zile nguzo.
Pia akatengeneza makomamanga 100, na
kuyashikamanisha kwenye minyororo.
17 Akazisimamisha hizo nguzo mbele ya
Hekalu, moja upande wa kusini na nyingine
upande wa kaskazini. Ile moja ya upande
wa kusini akaiita Yakini,[g] na ya upande wa
kaskazini akaiita Boazi.[h]

*Vifaa Vya Hekalu*

**(1 Wafalme 7:23-51)**

4 [i]Mfalme Solomoni akatengeneza
madhabahu ya shaba yenye urefu wa
dhiraa ishirini,[j] upana wa dhiraa ishirini na
kimo chake dhiraa kumi.[k] 2 [l]Akatengeneza
Bahari ya kusubu, yenye umbo la mviringo,
ya dhiraa kumi kutoka ukingo hadi ukingo
na kimo cha dhiraa tano. Kamba ya urefu
wa dhiraa thelathini[m] ingeweza kuizunguka.
3 [n]Chini ya huo ukingo, kulikuwa na
mafahali kuizunguka, yaani mafahali kumi
katika kila dhiraa moja.[o] Hayo mafahali
waliyasubu katika safu mbili yakiwa ya kitu
kimoja na hiyo Bahari.
4 [p]Bahari hiyo ilikaa juu ya mafahali kumi
na wawili, mafahali watatu walielekeza
nyuso zao kaskazini, watatu magharibi,
watatu kusini na watatu mashariki. Bahari
hiyo ilikaa juu ya hao mafahali, nazo
sehemu zao za nyuma zilielekeana. 5 [q]Unene
wake ulikuwa nyanda nne,[r] na ukingo wake
ulifanana na ukingo wa kikombe, kama
ua la yungiyungi iliyochanua. Iliweza
kuchukua bathi 3,000.[s]
6 [t]Kisha akatengeneza masinia kumi kwa
ajili ya kuoshea vifaa, naye akayaweka
matano upande wa kusini na matano
upande wa kaskazini. Ndani yake ndimo
walioshea vifaa vya kutumika katika sadaka
za kuteketezwa, lakini ile Bahari ilikuwa ni
kwa ajili ya makuhani kunawia.
7 [u]Akatengeneza vinara vya taa kumi vya
dhahabu kama ilivyoainishwa kwao na
kuviweka hekaluni, vinara vitano upande
wa kusini na vitano upande wa kaskazini.

---

[a]9 Shekeli 50 za dhahabu ni sawa na gramu 600.
[b]**3:10** Kut 25:18; 1Fal 6:23
[c]11 Dhiraa 5 ni sawa na mita 2.25.
[d]**3:14** Kut 26:31-33; Ebr 9:3; Mwa 3:24; Mt 27:51
[e]**3:15** 1Fal 7:15; Ufu 3:12; Yer 52:21
[f]**3:16** 1Fal 7:17-22
[g]17 Yakini maana yake Atathibitisha.
[h]17 Boazi maana yake Imo nguvu.
[i]**4:1** Eze 43:13; Kut 27:1-2; 2Fal 16:14; 1Fal 9:25
[j]1 Dhiraa 20 ni sawa na mita 9.
[k]1 Dhiraa 10 ni sawa na mita 4.5.
[l]**4:2** Kut 30:18; Ufu 4:6; 15:2; 1Fal 7:23
[m]2 Dhiraa 30 ni sawa na mita 13.5.
[n]**4:3** 1Fal 7:24
[o]3 Dhiraa moja ni sawa na sentimita 45.
[p]**4:4** Eze 48:30-34; Ufu 21:13
[q]**4:5** 1Fal 7:26
[r]5 Nyanda nne ni sawa na sentimita 7.5.
[s]5 Bathi 3,000 ni sawa na lita 60,000.
[t]**4:6** Kut 30:18; 1Fal 7:26; Ebr 9:9; 4:7
[u]**4:7** Kut 25:31, 40; 1Fal 7:49

8 [a]Akatengeneza meza kumi na kuziweka hekaluni, tano upande wa kusini na tano upande wa kaskazini. Pia akatengeneza mabakuli 100 ya dhahabu ya kunyunyizia.
9 [b]Akatengeneza ukumbi wa makuhani na ukumbi mwingine mkubwa na milango yake, naye akaifunika hiyo milango kwa
shaba. 10 Akaweka ile Bahari upande wa kusini, kwenye pembe ya kusini mashariki ya nyumba.
11 [c]Pia akatengeneza masufuria, masepetu na mabakuli ya kunyunyizia.

Kwa hiyo Huramu akakamilisha kazi katika Hekalu la Mungu kama vile Mfalme Solomoni alikuwa amemwagiza, yaani:

12 zile nguzo mbili;
yale mataji mawili yaliyokuwa juu ya hizo nguzo,
zile nyavu mbili za kupamba hayo mataji mawili yenye umbo la bakuli yaliyowekwa juu ya zile nguzo;
13 [d]yale makomamanga 400 kwa ajili ya hizo nyavu mbili (safu mbili za makomamanga kwa kila wavu yakipamba hayo mataji mawili yenye umbo la bakuli juu ya hizo nguzo);
14 [e]vishikio pamoja na masinia yake;
15 hiyo Bahari na hao mafahali kumi na wawili chini yake;
16 pia hayo masufuria, masepetu, uma za nyama na vyombo vingine vyote vilivyohusiana.

Vitu vyote ambavyo Huramu-Abi alimtengenezea Mfalme Solomoni kwa ajili ya Hekalu la BWANA vilikuwa vya shaba
iliyosuguliwa. 17 [f]Mfalme aliagiza wavisubu vitu hivi kwenye kalibu za udongo wa mfinyanzi katika uwanda wa Yordani kati ya Sukothi na Sereda.[g]
18 [h]Vitu hivi vyote Mfalme Solomoni alivyotengeneza vilikuwa vingi sana hivi kwamba uzito wa shaba haungekadirika.
19 [i]Solomoni pia akatengeneza samani zote zilizokuwa ndani ya Hekalu la Mungu:

madhabahu ya dhahabu;
meza za kuweka mikate ya Wonyesho;
20 [j]vinara vya taa vya dhahabu safi pamoja na taa zake ili ziwake mbele ya sehemu takatifu ya ndani kama ilivyoelekezwa;
21 [k]maua ya dhahabu yaliyofanyizwa, taa na makoleo (vilikuwa vya dhahabu bora kabisa);
22 [l]mikasi ya dhahabu safi, mabakuli ya kunyunyizia, masinia na vyetezo; milango ya dhahabu ya Hekalu: yaani milango ya ndani ya Patakatifu pa Patakatifu, na milango ya ukumbi mkuu.

5 [m]Hivyo Solomoni alipomaliza kazi ya Hekalu la BWANA, akaviingiza ndani vile vitu ambavyo Daudi baba yake alikuwa ameviweka wakfu: yaani, fedha, dhahabu na samani; kisha akaviweka katika hazina za Hekalu la Mungu.

*Sanduku La Agano Laletwa Hekaluni*

**(1 Wafalme 8:1-9)**

2 [n]Kisha Solomoni akawaita huko Yerusalemu wazee wa Israeli, viongozi wote wa makabila na wakuu wa jamaa za Waisraeli, ili walilete Sanduku la Agano la
BWANA kutoka Sayuni, Mji wa Daudi. 3 [o]Nao wanaume wote wa Israeli wakakusanyika

[a]**4:8** Kut 25:23; Hes 4:14; 1Fal 7:48-49
[b]**4:9** 2Fal 21:5; 2Nya 33:5
[c]**4:11** 1Fal 7:14
[d]**4:13** Yer 52:23; Wim 4:13; Kut 28:33-34; 1Fal 7:20
[e]**4:14** 1Fal 7:27-30
[f]**4:17** Mwa 33:17; 1Fal 7:46
[g]17 Au *Sarethani.*
[h]**4:18** 1Fal 7:23, 47
[i]**4:19** Kut 25:23, 30; 2Fal 24:13; Dan 5:2-3; Yer 28:3; 1Nya 28:6
[j]**4:20** Kut 27:20-21
[k]**4:21** Kut 37:20; 1Fal 6:18-35; Kut 25:31
[l]**4:22** Hes 7:14; Law 10:1; 1Fal 6:21
[m]**5:1** 1Fal 6:14; 2Sam 8:11; 1Nya 26:26-28; 22:14
[n]**5:2** 2Sam 6:12; 1Nya 15:25; 1Fal 8:1; 1Nya 29:1
[o]**5:3** 2Nya 7:8-10; 1Fal 8:2

kwa mfalme wakati wa sikukuu mwezi wa saba.

4 [a]Wazee wote wa Israeli walipofika, Walawi wakajitwika Sanduku la Agano, 5 [b]nao wakalipandisha Sanduku na Hema la Kukutania pamoja na vyombo vyote vitakatifu vilivyokuwa ndani yake. Makuhani, waliokuwa Walawi, walivibeba vitu hivyo, 6 naye Mfalme Solomoni na kusanyiko lote la Israeli waliokusanyika kumzunguka walikuwa mbele ya hilo Sanduku, nao wakatoa dhabihu nyingi za kondoo na ng'ombe ambao idadi yao haikuwezekana kuandikwa au kuhesabiwa.

7 [c]Makuhani wakalileta Sanduku la Agano la BWANA hadi mahali pake ndani ya sehemu takatifu ndani ya Hekalu, yaani Patakatifu pa Patakatifu, na kuliweka chini ya mabawa ya makerubi. 8 [d]Makerubi yalitandaza mabawa yao juu ya mahali pa Sanduku la Agano na kufunika Sanduku na mipiko yake ya kubebea. 9 [e]Mipiko hiyo ilikuwa mirefu sana kiasi kwamba ncha zake zilizojitokeza kutoka kwenye Sanduku, nazo zilionekana ukiwa mbele ya Patakatifu pa Patakatifu, lakini sio nje ya Mahali Patakatifu. Hiyo mipiko ipo hata leo. 10 [f]Ndani ya Sanduku hapakuwepo kitu kingine chochote isipokuwa zile mbao mbili ambazo Mose alikuwa ameziweka ndani yake huko Horebu, mahali ambapo BWANA alifanya Agano na Waisraeli baada ya kutoka Misri.

11 [g]Basi makuhani wakaondoka hapo Mahali Patakatifu. Makuhani wote waliokuwa huko walikuwa wamejiweka wakfu, bila kujali migawanyo yao. 12 [h]Walawi wote waliokuwa waimbaji, yaani, Asafu, Hemani, Yeduthuni, wana wa ndugu zao, walisimama upande wa mashariki wa madhabahu, wakiwa wamevaa kitani safi huku wakipiga matoazi, vinubi na zeze. Walikuwa pamoja na makuhani 120 wakipiga tarumbeta. 13 [i]Wapiga tarumbeta na waimbaji wakaungana katika sauti linganifu, ikawa kama vile ni sauti moja, wakimsifu na kumshukuru BWANA, nao alipoinua sauti zao pamoja na tarumbeta na matoazi na vyombo vingine vya uimbaji, wakamsifu BWANA wakisema:

"Yeye ni mwema;
upendo wake unadumu milele."

Ndipo Hekalu la BWANA likajazwa na wingu, 14 [j]nao makuhani hawakuweza kufanya huduma yao kwa sababu ya lile wingu, kwa kuwa utukufu wa BWANA ulijaza Hekalu la Mungu.

*Kuweka Hekalu Wakfu*

**(1 Wafalme 8:12-21)**

6 [k]Ndipo Solomoni akasema, "BWANA alisema kwamba ataishi katika giza nene. 2 [l]Nimejenga Hekalu zuri kwa ajili yako, mahali pako pa kukaa milele."

3 Kusanyiko lote la Israeli lilipokuwa limesimama hapo, mfalme akageuka na kuwabariki. 4 Kisha akasema:

"Ahimidiwe BWANA, Mungu wa Israeli, ambaye kwa mikono yake mwenyewe ametimiza lile alilomwahidi Daudi baba yangu kwa kinywa chake mwenyewe. Kwa kuwa alisema, 5 'Tangu siku niliyowatoa watu wangu kutoka Misri, sikuchagua mji katika kabila lolote la Israeli ili Hekalu lijengwe humo ili Jina langu lipate kuwamo humo, wala sikumchagua mtu yeyote kuwa kiongozi wa watu wangu Israeli. 6 [m]Lakini sasa nimeuchagua Yerusalemu

[a]**5:4** Yos 3:6
[b]**5:5** Hes 3:31; 1Nya 15:2
[c]**5:7** Ufu 11:19
[d]**5:8** Mwa 3:24
[e]**5:9** 1Fal 8:8
[f]**5:10** Ebr 9:4; Kum 10:2; Kut 16:34; 2Nya 6:11
[g]**5:11** 1Nya 24:1
[h]**5:12** 1Nya 15:16-24; 9:33
[i]**5:13** 1Nya 16:34; Yer 33:11; Za 106:1; 2Nya 7:3; Za 136:1-6
[j]**5:14** Kut 40:35; 19:16; 2Nya 7:2-3; Ufu 15:8; Hes 19:5; Isa 6:4; Eze 43:4; Hag 2:7; 2Kor 3:11
[k]**6:1** 1Fal 8:12; Kut 19:9; Law 16:2; Ebr 12:18; Kut 20:21; 24:15-18; Za 18:8-11
[l]**6:2** Ezr 7:15; Za 135:21
[m]**6:6** Za 78:68-70; Kum 12:5; Kut 20:24; 2Nya 12:13; 1Nya 28:4; 1Sam 16:1; Za 89:19-20

ili Jina langu lipate kuwamo humo, na
nimemchagua Daudi kuwatawala watu
wangu Israeli.’
7 [a]“Ilikuwa moyoni mwa Daudi baba
yangu kujenga Hekalu kwa ajili ya Jina
la BWANA, Mungu wa Israeli. 8 [b]Lakini
BWANA akamwambia Daudi baba
yangu, ‘Kwa sababu ilikuwa moyoni
mwako kujenga Hekalu kwa ajili ya
Jina langu, ulifanya vyema kuwa na
jambo hili moyoni mwako. 9 Hata
hivyo, sio wewe utakayenijengea
Hekalu, bali mwanao, ambaye ni
nyama yako na damu yako mwenyewe,
yeye ndiye atakayejenga Hekalu kwa
ajili ya Jina langu.’
10 “BWANA ametimiza ahadi
aliyoiweka: Nimeingia mahali pa Daudi
baba yangu na sasa ninakikalia kiti cha
ufalme cha Israeli, kama vile BWANA
alivyoahidi, nami nimejenga Hekalu
kwa ajili ya Jina la BWANA, Mungu wa
Israeli. 11 [c]Nimeliweka humo Sanduku
la Agano, ambamo ndani yake kuna lile
Agano la BWANA alilofanya na watu
wa Israeli.”

*Maombi Ya Solomoni Ya Kuweka Wakfu*

**(1 Wafalme 8:22-53)**

12 [d]Kisha Solomoni akasimama mbele
ya madhabahu ya BWANA machoni pa
kusanyiko lote la Israeli, naye akakunjua
mikono yake. 13 [e]Basi Solomoni alikuwa
ametengeneza jukwaa la shaba, urefu wake
dhiraa tano, na upana wake dhiraa tano na
kimo chake dhiraa tatu, naye akaliweka
katikati ya ukumbi wa nje. Akapanda juu
ya hilo jukwaa kisha akapiga magoti mbele
ya kusanyiko lote la Israeli, akanyoosha
mikono yake kwelekea mbinguni.
14 [f]Akasema:

“Ee BWANA, Mungu wa Israeli,
hakuna Mungu kama wewe juu
mbinguni wala chini duniani, wewe
unayetunza Agano lako la upendo na
watumishi wanaodumu katika njia
yako kwa moyo wote. 15 [g]Umetimiza
ahadi yako kwa mtumishi wako Daudi
baba yangu, kwa kinywa chako uliahidi
na kwa mkono wako umetimiza, kama
ilivyo leo.
16 [h]“Sasa BWANA, Mungu wa Israeli,
mtimizie mtumishi wako Daudi baba
yangu ahadi zako ulizomwahidi
uliposema, ‘Kamwe hutakosa kuwa na
mtu atakayeketi mbele zangu kwenye
kiti cha ufalme cha Israeli, kama
wanao wakiangalia yote wayafanyayo
kuenenda mbele zangu kama vile
ulivyofanya.’ 17 Sasa, Ee BWANA,
Mungu wa Israeli, acha neno lako lile
ulilomwahidi mtumishi wako Daudi
baba yangu litimie.
18 [i]“Lakini kweli, je, Mungu atafanya
makao duniani na wanadamu? Mbingu,
hata mbingu zilizo juu sana, haziwezi
kukutosha wewe. Sembuse Hekalu hili
nililojenga! 19 Hata hivyo sikiliza dua ya
mtumishi wako na maombi yake kwa
huruma, Ee BWANA Mungu wangu.
Sikia kilio na dua ambayo mtumishi
wako anaomba mbele zako siku hii
ya leo. 20 [j]Macho yako na yafumbuke
kuelekea Hekalu hili usiku na mchana,
mahali hapa ambapo ulisema, ‘Jina
langu litakuwako humo,’ ili kwamba
upate kusikia maombi ambayo
mtumishi wako ataomba kuelekea
mahali hapa. 21 [k]Usikie maombi ya
mtumishi wako na ya watu wako
Israeli wakati wanapoomba kuelekea
mahali hapa. Sikia kutoka mbinguni,
mahali pa makao yako na usikiapo,
samehe.

[a]**6:7** 2Sam 7:2; 1Nya 28:2; Mdo 7:46; 1Fal 7:3
[b]**6:8** 1Fal 8:18-21; 2Kor 8:12
[c]**6:11** Kut 40:20; 10:2; Za 50:5; 1Fal 8:9-21; 2Nya 5:10
[d]**6:12** 1Fal 8:22; Ebr 9:5; 1Tim 2:8
[e]**6:13** Neh 8:4; Za 95:6
[f]**6:14** Kut 15:11; 8:10; Mwa 5:24; Kum 7:9; Dan 9:4; 2Sam 7:22; Za 86:8
[g]**6:15** 1Nya 22:9-10
[h]**6:16** 1Fal 2:4; 2Nya 7:18; Za 132:12; 2Sam 7:12-16; 1Fal 6:12
[i]**6:18** Ufu 21:3; Isa 40:22; Mdo 7:49; Za 113:5-6; 2Nya 2:6
[j]**6:20** Dan 6:10; Kut 3:16; Kum 12:11; 2Nya 7:14; 30:20; Za 33:18; 34:15
[k]**6:21** Isa 43:25; 55:7; Mik 7:18; Isa 44:22

22 [a]“Mtu anapomkosea jirani yake
na akatakiwa kuapa, akija na kuapa
mbele ya madhabahu yako ndani
ya Hekalu hili, 23 [b]basi, sikia kutoka
mbinguni na ukatende. Hukumu kati
ya watumishi wako, ukimwadhibu
yule mwenye hatia kwa kuleta juu
ya kichwa chake yale aliyoyatenda.
Umtangazie mwenye haki kwamba
hana hatia, hivyo ukathibitishe kuwa
haki kwake.

24 [c]“Wakati watu wako Israeli
watakapokuwa wameshindwa na adui
kwa sababu ya dhambi walizofanya
dhidi yako, watakapokugeukia na
kulikiri jina lako, wakiomba na
kufanya dua kwako katika Hekalu
hili, 25 basi usikie kutoka mbinguni,
ukasamehe dhambi ya watu wako
Israeli na kuwarudisha katika nchi
uliyowapa baba zao.

26 [d]“Wakati mbingu zitakapokuwa
zimefungwa kusiwe na mvua kwa
sababu watu wako wametenda dhambi
dhidi yako, watakapoomba kuelekea
mahali hapa na kulikiri jina lako nao
wakageuka kutoka dhambi zao kwa
sababu umewaadhibu, 27 [e]basi usikie
kutoka mbinguni na usamehe dhambi
ya watumishi wako, watu wako Israeli.
Wafundishe njia sahihi ya kuishi na
ukanyeshe mvua juu ya nchi uliyowapa
watu wako kuwa urithi.

28 [f]“Wakati njaa au tauni vikija juu ya
nchi, au koga au kawa, nzige au panzi,
au wakati adui atakapowazingira
katika mji wao wowote, maafa ya
namna yoyote au ugonjwa wowote
unaoweza kuwajia, 29 wakati dua
au maombi yatakapofanywa na
mmojawapo wa watu wako Israeli,
kila mmoja akitambua taabu zake
na uchungu wake, naye akainyoosha
mikono yake kuelekea Hekalu hili,
30 [g]basi usikie kutoka mbinguni, katika
makao yako. Usamehe na utende,
umpe kila mtu kulingana na matendo
yake, kwa kuwa unaujua moyo wake
(kwa kuwa ni wewe peke yako ujuaye
mioyo ya watu wote), 31 [h]ili wakuogope
kwa wakati wote watakaoishi katika
nchi uliyowapa baba zetu.

32 [i]“Kwa habari ya mgeni ambaye
si miongoni mwa watu wako Israeli,
lakini amekuja kutoka nchi ya mbali
kwa sababu ya jina lako kuu na mkono
wako wenye nguvu ulionyooshwa,
atakapokuja kuomba kuelekea
Hekalu hili, 33 [j]basi na usikie kutoka
mbinguni, mahali pa makao yako,
ukafanye lolote ambalo mgeni huyo
anakuomba, ili mataifa yote ya dunia
wapate kujua jina lako na wakuogope
kama wafanyavyo watu wako Israeli
nao wapate pia kujua kwamba nyumba
hii niliyoijenga imeitwa kwa Jina lako.

34 [k]“Wakati watu wako
watakapokwenda vitani dhidi ya
adui zao, popote utakapowapeleka,
wakati watakapoomba kwa BWANA
kuelekea mji ambao umeuchagua, na
Hekalu nililolijenga kwa ajili ya Jina
lako, 35 basi usikie dua na maombi yao
kutoka mbinguni, ukawatetee haki
yao.

36 [l]“Watakapotenda dhambi dhidi
yako, kwa kuwa hakuna mtu yeyote
ambaye hatendi dhambi, nawe
ukachukizwa nao na kuwakabidhi
kwa adui, ambaye atawachukua
utumwani katika nchi iliyo mbali au

---

[a]**6:22** Kut 22:11
[b]**6:23** Isa 3:11; Rum 2:8; Mt 16:27
[c]**6:24** Law 26:17; Kum 32:15; Amu 2:11-15; Za 51:4
[d]**6:26** 2Sam 1:21; Lk 4:25; 1Fal 17:1; Law 26:10
[e]**6:27** 2Nya 7:14; Yn 6:45; Zek 10:1; 1Fal 8:35, 36; Za 94:12
[f]**6:28** 2Nya 20:9
[g]**6:30** 1Sam 2:3; 1Nya 28:9; Za 11:4
[h]**6:31** Kum 6:13; Za 34:7-9
[i]**6:32** 2Nya 9:6; Kum 4:6-8; Yn 12:20; Mdo 8:27; Kut 3:19-20; Kum 4:6-8; Za 113:3; Isa 56:3-8; Yn 10:16
[j]**6:33** Kut 12:43; 2Nya 7:14
[k]**6:34** Kum 28:7; 1Nya 5:20
[l]**6:36** 1Fal 8:46; Law 26:44; Rum 3:9; Ay 15:14-16; Mit 20:9; Mhu 7:20; Yak 3:2

karibu [37] [a]na kama watabadilika mioyo
yao katika nchi wanakoshikiliwa
mateka, nao wakatubu na kukulilia
katika nchi ya utumwa na kusema,
'Tumetenda dhambi, tumefanya
makosa na tumetenda uovu'; [38] [b]kama
wakikugeukia kwa moyo wao wote na
nafsi zao katika nchi ya adui zao ambao
waliwachukua mateka, wakakuomba
kuelekea nchi uliyowapa baba zao,
kuelekea mji uliouchagua na Hekalu
nililolijenga kwa ajili ya Jina lako,
[39] basi kutoka mbinguni, mahali pa
makao yako, usikie dua yao na maombi
yao na kuitetea haki yao. Uwasamehe
watu wako, waliotenda dhambi dhidi
yako.

[40] [c]"Sasa, Mungu wangu, macho yako
na yafumbuke na masikio yako yasikie
maombi yaombwayo mahali hapa.

[41] [d]"Sasa inuka, Ee Bwana Mungu,
na uje mahali pako pa
kupumzikia,
wewe na Sanduku la nguvu zako.
Makuhani wako, Ee Bwana Mungu,
na wavikwe wokovu,
watakatifu wako na wafurahi
katika wema wako.
[42] [e]Ee Bwana Mungu, usimkatae
mpakwa mafuta wako.
Kumbuka upendo mkuu
uliomwahidia
Daudi mtumishi wako."

*Hekalu Lawekwa Wakfu*

**(1 Wafalme 8:62-66)**

7 [f]Baada ya Solomoni kumaliza kuomba,
moto ukashuka kutoka mbinguni na
kuteketeza sadaka ya kuteketezwa na
dhabihu, nao utukufu wa Bwana ukalijaza
Hekalu. [2] [g]Makuhani hawakuweza kuingia
ndani ya Hekalu la Bwana kwa sababu
utukufu wa Bwana ulilijaza. [3] [h]Waisraeli
wote walipoona moto ukishuka na utukufu
wa Bwana ukiwa juu ya Hekalu, wakapiga
magoti sakafuni wakasujudu nyuso zao
mpaka chini, nao wakamwabudu na
kumshukuru Bwana wakisema,

"Yeye ni mwema;
upendo wake unadumu milele."

[4] [i]Ndipo mfalme na watu wote wakatoa
dhabihu mbele za Bwana Mungu. [5] Naye
Mfalme Solomoni akatoa dhabihu ya
ng'ombe 22,000 pamoja na kondoo na
mbuzi 120,000. Hivyo ndivyo mfalme na
watu wote walivyoweka wakfu Hekalu la
Mungu. [6] [j]Makuhani wakasimama kwenye
nafasi zao, vivyo hivyo Walawi wakiwa na
vyombo vya uimbaji vya Bwana ambavyo
Mfalme Daudi alikuwa ametengeneza kwa
ajili ya kumsifu Bwana, navyo vilitumika
wakati aliposhukuru, akisema, "Upendo
wake wadumu milele." Mkabala na Walawi,
makuhani walipiga tarumbeta zao, nao
Waisraeli wote walikuwa wamesimama.

[7] [k]Solomoni akaweka wakfu sehemu ya
katikati ya ua uliokuwa mbele ya Hekalu
la Bwana na hapo akatoa sadaka za
kuteketezwa na mafuta ya sadaka za amani,
kwa sababu madhabahu ya shaba aliyokuwa
ametengeneza haikutosha kuweka sadaka
hizo zote za kuteketezwa, sadaka za nafaka
na za mafuta.

[8] [l]Hivyo Solomoni akaiadhimisha sikukuu
wakati ule kwa muda wa siku saba, na
Israeli wote pamoja naye. Walikuwa
kusanyiko kubwa sana, watu kutoka Lebo-
Hamathi hadi Kijito cha Misri. [9] [m]Katika siku
ya nane walifanya kusanyiko, kwa kuwa

[a]**6:37** 1Fal 8:48; Isa 58:3; Yer 24:6-7
[b]**6:38** Yer 29:12-13
[c]**6:40** Za 130:2; Isa 37:17
[d]**6:41** Isa 33:10; Neh 9:25; Isa 51:10; Za 132:16; 1Nya 28:2
[e]**6:42** Za 89:24-28; Isa 55:3
[f]**7:1** Kut 19:18; Mwa 15:17; Law 9:24; Kut 16:10; Dan 9:20; 1Fal 8:54; Isa 65:24; Mdo 4:31; Amu 6:21; 1Fal 18:38; 1Nya 21:26; 2Nya 5:13; Eze 10:3; Ufu 21:23
[g]**7:2** 2Nya 5:14; Kut 29:43; 1Fal 8:11
[h]**7:3** 1Nya 16:34; Ezr 3:11; 2Nya 5:13; 20:13; 20:21; Za 103:17
[i]**7:4** 1Fal 8:62
[j]**7:6** 1Nya 15:16-24; 2Nya 5:12
[k]**7:7** Hes 16:37; 2Nya 36:14; Ebr 13:10-12; 1Fal 8:64
[l]**7:8** 2Nya 30:26; Mwa 15:18; Neh 8:17; Yos 13:3
[m]**7:9** Law 23:36

walikuwa wanaadhimisha kuwekwa wakfu
kwa madhabahu kwa muda wa siku saba na
sikukuu kwa muda wa siku nyingine saba
zaidi. 10 Katika siku ya ishirini na tatu ya
mwezi wa saba Solomoni akawaaga watu
waende nyumbani mwao, wakishangilia
na kufurahi mioyoni mwao, kwa wema
mwingi BWANA Mungu aliomtendea Daudi
na Solomoni na kwa ajili ya watu wake
Israeli.

*BWANA Mungu Amtokea Solomoni*

**(1 Wafalme 9:1-9)**

11 Solomoni alipomaliza kujenga Hekalu
la BWANA na jumba la kifalme, naye akiwa
amefanikiwa kutenda yale yote aliyokuwa
nayo moyoni mwake kufanya katika Hekalu
la BWANA na katika jumba lake mwenyewe
la kifalme, 12 [a]BWANA akamtokea Solomoni
usiku na kumwambia:

"Nimesikia maombi yako nami
nimechagua mahali hapa kwa ajili
yangu mwenyewe kuwa Hekalu kwa
ajili ya dhabihu.
13 [b]"Wakati nitakapofunga mbingu
ili isiwepo mvua, au nikiamuru nzige
kula mazao ya nchi au nikituma tauni
miongoni mwa watu wangu, 14 [c]kama
watu wangu, wanaoitwa kwa Jina
langu, watajinyenyekesha na kuomba
na kuutafuta uso wangu na kuacha
njia zao mbaya, basi nitasikia toka
mbinguni na kuwasamehe dhambi
yao na nitaiponya nchi yao. 15 [d]Sasa
macho yangu yatafumbuka na masikio
yangu yatasikiliza kwa makini maombi
yaombwayo mahali hapa. 16 [e]Kwa
maana sasa nimechagua na kutakasa
Hekalu hili ili kwamba Jina langu
lipate kuwa huko milele. Macho yangu
na moyo wangu utakuwepo huko
daima.
17 [f]"Kwa habari yako wewe, kama
ukienenda mbele zangu kama Daudi
baba yako alivyoenenda na kufanya
yote nikuamuruyo, nawe ukizishika
amri zangu na sheria zangu,
18 [g]Nitakiimarisha kiti chako cha enzi
kama nilivyoagana na Daudi baba yako
niliposema, 'Hutakosa kamwe mtu wa
kutawala juu ya Israeli.'
19 [h]"Lakini kama ukigeuka na
kuyaacha maagizo na amri nilizowapa
na kwenda kuitumikia miungu
mingine na kuiabudu, 20 [i]ndipo
nitakapoing'oa Israeli kutoka nchi
yangu niliyowapa, nami nitalikataa
Hekalu hili nililolitakasa kwa ajili
ya Jina langu. Nitalifanya kitu cha
kudharauliwa na kitu cha kudhihakiwa
miongoni mwa watu wote. 21 [j]Ingawa
Hekalu hili linavutia sana sasa,
wote watakaolipita watashangaa na
kusema, 'Kwa nini BWANA amefanya
kitu kama hiki katika nchi hii na kwa
Hekalu hili?' 22 [k]Watu watajibu, 'Ni
kwa sababu wamemwacha BWANA,
Mungu wa baba zao, aliyewatoa Misri,
nao wamekumbatia miungu mingine,
wakaiabudu na kuitumikia, ndiyo
sababu ameyaleta maafa haya yote
juu yao.' "

*Shughuli Nyingine Za Solomoni*

**(1 Wafalme 9:10-28)**

8 [l]Miaka ishirini ilipopita, ambayo katika
hiyo Solomoni alilijenga Hekalu la
BWANA na jumba lake mwenyewe la
kifalme, 2 Solomoni akajenga tena vijiji
vile ambavyo Hiramu alikuwa amempa,
naye akawapa Waisraeli waishi humo.

[a]**7:12** Kum 12:5; Mwa 12:7; Za 78:68-69
[b]**7:13** 2Nya 6:26; Kum 11:17; Amo 4:7
[c]**7:14** Yak 4:10; Eze 18:32; Kut 10:3; 1Nya 16:11; Kut 15:26; 2Nya 6:27
[d]**7:15** 1Fal 8:29; 2Nya 6:40; Neh 1:6
[e]**7:16** Kum 12:5; 2Nya 6:6
[f]**7:17** 1Fal 9:4
[g]**7:18** Mik 5:2; 2Sam 17:13; 1Nya 17:12; 2Nya 6:16
[h]**7:19** Kum 28:15; Law 26:14, 33
[i]**7:20** Kum 28:37; 29:28; 1Fal 14:15; Yer 12:14; 16:13; 50:11; Za 5:5
[j]**7:21** Kum 29:24; Yer 22:8; Mao 2:15; Yer 7:14
[k]**7:22** Amu 2:13; Dan 9:12; 2Fal 17:18; 2Nya 36:16
[l]**8:1** 1Fal 9:10

3 [a]Kisha Solomoni akaenda Hamath-Soba
na kuuteka. 4 [b]Pia akajenga mji wa Tadmori
katika jangwa na miji yote ya kuhifadhia
vitu katika Hamathi. 5 [c]Akajenga tena Beth-
Horoni ya Juu na Beth-Horoni ya Chini, miji
yenye ngome, kuta, malango na makomeo.
6 [d]Solomoni pia akajenga Baalathi na miji
yake yote ya kuhifadhia vitu, na miji kwa
ajili ya magari yake na kwa ajili ya farasi
wake, chochote alichotaka kujenga katika
Yerusalemu, katika Lebanoni na katika nchi
yote aliyotawala.

7 [e]Watu wote waliosalia kutoka kwa
Wahiti, Waamori, Waperizi, Wahivi
na Wayebusi (haya mataifa hayakuwa
Waisraeli), 8 [f]yaani, wazao wao waliobakia
katika nchi, ambao Waisraeli hawakuwa
wamewaangamiza: hawa Solomoni
akawalazimisha kuwa watumwa katika
shokoa, kama ilivyo hadi leo. 9 [g]Lakini
Solomoni hakuwafanya Waisraeli watumwa
kwa ajili ya kazi yake, bali walikuwa
wapiganaji, majemadari, maafisa wake,
majemadari wa magari yake ya vita na
waendesha magari ya vita. 10 [h]Pia walikuwa
maafisa wakuu wa Mfalme Solomoni, yaani,
maafisa wakaguzi 250 waliosimamia watu.

11 [i]Solomoni akampandisha mke wake
binti Farao kutoka Mji wa Daudi na kumleta
jumba la kifalme alilokuwa amemjengea,
kwa kuwa alisema, “Mke wangu hataishi
katika jumba la kifalme la Daudi mfalme
wa Israeli, kwa sababu mahali ambapo
Sanduku la Bwana limefika ni patakatifu.”

12 [j]Mfalme Solomoni akamtolea Bwana
dhabihu za kuteketezwa juu ya madhabahu
ya Bwana ambayo alikuwa ameijenga
mbele ya ukumbi, 13 [k]kulingana na mahitaji
ya kila siku kwa ajili ya sadaka zilizoamriwa
na Mose kwa ajili ya Sabato, Mwezi
Mwandamo na sikukuu nyingine tatu za
mwaka, yaani, Sikukuu ya Mikate Isiyotiwa
Chachu, Sikukuu ya Majuma na Sikukuu
ya Vibanda. 14 [l]Kwa kushika maagizo ya
Daudi baba yake, aliweka migawanyo ya
makuhani kwa ajili ya kazi zao, nao Walawi
kuongoza kusifu na kusaidia makuhani
kufuatana na mahitaji ya kila siku. Pia
akaweka mabawabu katika migawanyo kwa
ajili ya malango mbalimbali, kwa sababu
hili ndilo Daudi mtu wa Mungu alilokuwa
ameagiza. 15 Nao hawakuziacha amri za
mfalme alizoamuru makuhani au Walawi
katika jambo lolote, ikiwa ni pamoja na
zile za hazina.

16 Kazi yote ya Mfalme Solomoni ilifanyika
kuanzia siku msingi wa Hekalu la Bwana
ulipowekwa mpaka kukamilika kwake.
Kwa hiyo Hekalu la Bwana likamalizika
kujengwa.

17 [m]Ndipo Solomoni akaenda Esion-Geberi
na Elathi katika pwani ya Edomu. 18 [n]Naye
Hiramu alimpelekea meli zilizoongozwa na
maafisa wake mwenyewe, watu waliokuwa
na ujuzi wa baharini. Hawa watu pamoja
na wale wa Solomoni wakasafiri kwa bahari
mpaka Ofiri, wakaleta kutoka huko talanta
450 za dhahabu, ambazo walimkabidhi
Mfalme Solomoni.

### *Malkia Wa Sheba Amtembelea Solomoni*

**(1 Wafalme 10:1-13)**

9 [o]Malkia wa Sheba aliposikia habari za
umaarufu wa Solomoni, huyo malkia
akaja Yerusalemu kumjaribu kwa maswali
magumu. Alifika akiwa na msafara mkubwa
sana, pamoja na ngamia waliobeba

---

[a]**8:3** Hes 13:21; 2Sam 8:2-3
[b]**8:4** 1Fal 9:14
[c]**8:5** Yos 10:10; 1Nya 7:24; Hes 13:21
[d]**8:6** Yos 15:11
[e]**8:7** Mwa 15:18-21; 1Fal 9:20; Ezr 9:1; Mwa 10:15
[f]**8:8** 1Fal 9:21; 2Nya 2:18
[g]**8:9** Kut 19:5; Kum 23:19; Law 25:39; Gal 4:28-31
[h]**8:10** 1Fal 5:16; 9:23; 2Nya 2:18
[i]**8:11** 1Fal 7:8; 9:24
[j]**8:12** 1Fal 8:64; 1Nya 4:1
[k]**8:13** Kut 29:38; Hes 28:3-9; Kut 23:14-16; Kum 16:16; 1Fal 9:25
[l]**8:14** 1Nya 24:1; 9:17; Neh 12:24, 36, 45; 1Nya 23:6; 2Sam 23:2; 2Nya 5:11; 31:2; 1Nya 25:1; 26:1
[m]**8:17** Kum 2:8; 2Fal 14:22; 1Fal 9:26
[n]**8:18** 1Fal 9:27; Isa 13:12; 2Nya 9:9; Mwa 10:29; Ay 22:24
[o]**9:1** Mwa 10:7; Eze 20:49; Lk 11:31; Mt 12:42; 13:11, 35; Za 49:4; 78:2; Mit 1:5

vikolezi, kiasi kikubwa cha dhahabu na
vito vya thamani, alikuja kwa Solomoni
na kuzungumza naye kuhusu yote ambayo
alikuwa nayo moyoni mwake. 2 Solomoni
akamjibu maswali yake yote, wala
hakukuwa na jambo lolote lililokuwa gumu
kwake asiweze kumwelezea. 3 [a]Malkia wa
Sheba alipoona hekima yote ya Solomoni
na jumba la kifalme alilokuwa amejenga,
4 chakula kilichokuwa mezani pake, jinsi
maafisa wake walivyokaa, wahudumu
katika majoho yao, wanyweshaji wake
na sadaka za kuteketezwa alizotoa katika
Hekalu la BWANA alipatwa na mshangao.
5 Akamwambia mfalme, "Taarifa
niliyosikia kwenye nchi yangu mwenyewe
kuhusu mafanikio na hekima yako ni kweli.
6 [b]Lakini sikuamini yaliyosemwa hadi
nilipokuja na kuona kwa macho yangu
mwenyewe. Naam, sikuambiwa hata nusu
yake; katika hekima na mali umezidi sana
kuliko ile taarifa niliyoisikia. 7 Heri watu
wako! Heri hawa maafisa wako wasimamao
mbele yako daima na kusikia hekima yako!
8 [c]Ahimidiwe BWANA Mungu wako, ambaye
amependezwa sana nawe, na akakuweka
juu ya kiti chake cha ufalme utawale kwa
niaba ya BWANA Mungu wako. Kwa sababu
ya upendo wa Mungu wako kwa Israeli na
shauku yake ya kuwadhibitisha milele,
amekufanya wewe mfalme juu yao, ili
kudumisha haki na uadilifu."
9 [d]Naye akampa mfalme talanta 120[e] za
dhahabu, kiasi kikubwa cha vikolezi na vito
vya thamani. Haikuwahi kamwe kuletwa
vikolezi vizuri kama vile Malkia wa Sheba
alivyompa Mfalme Solomoni.
10 [f](Watumishi wa Hiramu na wa
Solomoni wakaleta dhahabu kutoka Ofiri,
tena wakaleta shehena kubwa ya miti ya
msandali na vito vya thamani. 11 Mfalme
akatumia hiyo miti ya msandali kuwa ngazi
kwa ajili ya Hekalu la BWANA na kwa jumba
la kifalme, pia kwa kutengeneza vinubi na
zeze kwa ajili ya waimbaji. Kiasi hicho kingi
cha msandali hakijawahi kuingizwa Yuda
tangu siku ile.)
12 Mfalme Solomoni akampa Malkia wa
Sheba kila kitu alichotamani na kukiomba,
zaidi ya vile alivyokuwa amemletea mfalme.
Kisha malkia akaondoka na kurudi katika
nchi yake, yeye na watumishi wake.

*Fahari Ya Solomoni*

**(1 Wafalme 10:14-25)**

13 Uzito wa dhahabu ambayo Solomoni
alipokea kwa mwaka ulikuwa talanta
666,[g] 14 [h]mbali na mapato yaliyoletwa na
wafanyabiashara na wachuuzi. Wafalme
wote wa Arabuni na watawala wa nchi
wakamletea Solomoni dhahabu na fedha.
15 Mfalme Solomoni akatengeneza ngao
kubwa 200 kwa dhahabu iliyofuliwa. Kila
ngao ilikuwa na dhahabu yenye uzito wa
shekeli 600[i] 16 [j]Akatengeneza pia ngao
ndogo 300 za dhahabu iliyofuliwa, kila
ngao ikiwa na uzito wa mane tatu[k] za
dhahabu. Mfalme akaziweka katika Jumba
la Kifalme la Msitu wa Lebanoni.
17 [l]Kisha mfalme akatengeneza kiti
kikubwa cha kifalme kwa kutumia pembe
za ndovu na kukifunika kwa dhahabu
safi. 18 Kiti hicho kilikuwa na ngazi sita
na mahali pa kuwekea miguu vyote vya
dhahabu. Pande zote za kiti kulikuwa na
mahali pa kuegemeza mikono, na simba
wawili wakisimama kando ya hiyo mikono.
19 Simba kumi na wawili walisimama
kwenye ngazi sita, mmoja katika kila
upande wa kila ngazi. Hakuna kitu kama
hicho kilichokuwa kimefanyika kwenye
ufalme mwingine wowote. 20 Vikombe
vyote vya Mfalme Solomoni vya kunywea

[a]**9:3** 1Fal 5:12
[b]**9:6** 2Nya 6:32
[c]**9:8** 1Fal 2:12; 1Nya 28:5; Za 72:8-9
[d]**9:9** 2Nya 8:18
[e]9 Talanta 120 za dhahabu ni sawa na tani 4.5.
[f]**9:10** 1Fal 5:2-6; 2Nya 8:18; 1Fal 9:27-28; 10:11; Za 72:10
[g]13 Talanta 666 za dhahabu ni sawa na tani 25.
[h]**9:14** Isa 21:13; Eze 27:21; Yer 25:24; Isa 45:14; Za 68:29; 72:10; Isa 60:6
[i]15 Shekeli 600 za dhahabu ni sawa na kilo 3.5.
[j]**9:16** 2Nya 12:9; 1Fal 7:2
[k]16 Mane tatu za dhahabu ni sawa na kilo 1.7.
[l]**9:17** 1Fal 22:39

vilikuwa vya dhahabu na vyombo vyote
vya nyumbani katika Jumba la Kifalme la
Msitu wa Lebanoni vilikuwa vya dhahabu
safi. Hakukuwa na kitu kilichotengenezwa
kwa fedha, kwa sababu fedha ilionekana
ya thamani ndogo wakati wa Solomoni.
21 [a]Mfalme alikuwa na meli nyingi za
biashara[b] baharini zilizoendeshwa na watu
wa Hiramu. Kwa mara moja kila miaka
mitatu zilirudi, zikiwa zimebeba dhahabu,
fedha, pembe za ndovu na nyani wakubwa
na wadogo.

22 [c]Mfalme Solomoni alikuwa mkuu zaidi
kwa utajiri na hekima kuliko wafalme
wote wa dunia. 23 [d]Wafalme wote wa
dunia wakatafuta kukutana na Solomoni
ili kusikia hekima ambayo Mungu alikuwa
ameiweka katika moyo wake. 24 [e]Mwaka
baada ya mwaka, kila mmoja ambaye
alikuja, alileta zawadi, vyombo vya fedha
na dhahabu, majoho, silaha na vikolezi,
farasi na nyumbu.

25 [f]Solomoni alikuwa na mabanda 4,000
kwa ajili ya farasi na magari ya vita, farasi
12,000 ambao aliwaweka katika miji ya
magari ya vita na katika Yerusalemu
pamoja naye. 26 [g]Solomoni akatawala juu
ya wafalme wote kuanzia Mto Frati mpaka
kwenye nchi ya Wafilisti na kuendelea
hadi mpaka wa Misri. 27 [h]Mfalme akafanya
fedha kuwa kitu cha kawaida kama mawe
huko Yerusalemu, mierezi akaifanya kuwa
mingi kama mikuyu vilimani. 28 [i]Farasi wa
Solomoni waliletwa kutoka Misri na kutoka
nchi nyingine zote.

*Kifo Cha Solomoni*

**(1 Wafalme 11:41-43)**

29 [j]Kwa habari za matukio mengine ya
utawala wa Solomoni, kuanzia mwanzo
hadi mwisho, je, hayakuandikwa katika
kumbukumbu za nabii Nathani, katika
unabii wa Ahiya Mshiloni na katika maono
ya Ido mwonaji kuhusu Yeroboamu mwana
wa Nebati? 30 [k]Solomoni alitawala Israeli
yote miaka arobaini, akiwa Yerusalemu.
31 [l]Kisha Solomoni akalala pamoja na baba
zake, naye akazikwa katika mji wa Daudi
baba yake. Naye Rehoboamu mwanawe
akawa mfalme baada yake.

*Israeli Wanamwasi Rehoboamu*

**(1 Wafalme 12:1-20)**

10 [m]Rehoboamu akaenda Shekemu,
kwa kuwa Waisraeli wote walikuwa
wamekwenda huko kumfanya yeye kuwa
mfalme. 2 [n]Yeroboamu mwana wa Nebati
aliposikia hili (alikuwa bado yuko Misri
alikokuwa amekimbilia awe mbali na
Mfalme Solomoni), akarudi kutoka Misri.
3 Kwa hiyo wakatuma watu kumwita
Yeroboamu, yeye na kusanyiko lote la
Israeli wakamwendea Rehoboamu na
kumwambia, 4 [o]"Baba yako aliweka nira
nzito, lakini sasa tupunguzie kazi za kikatili
na nira nzito aliyoweka juu yetu, nasi
tutakutumikia."

5 Rehoboamu akajibu, "Nendeni kwa
muda wa siku tatu na kisha mnirudie." Basi
watu wakaenda zao.

6 [p]Kisha Mfalme Rehoboamu akataka
shauri kwa wazee ambao walimtumikia
Solomoni baba yake wakati wa uhai wake
akawauliza, "Mnanishauri nini katika
kuwajibu watu hawa?"

7 [q]Wakajibu, "Kama leo utakuwa mtumishi

---

[a]**9:21** 1Fal 10:22; Isa 2:16; Yer 10:9; Yn 1:3; 1Fal 22:48; Za 48:7; Isa 60:9; Za 72:10
[b]21 Au: za Tarshishi (ona pia 1Fal 10:22; 22:48; 2Nya 20:36; Isa 2:16; 60:9).
[c]**9:22** 1Fal 3:13; 2Nya 1:12; Kol 2:2-3; Mt 12:42; 1Fal 10:23-24; Za 89:27
[d]**9:23** 1Fal 4:34
[e]**9:24** Za 45:12; Isa 18:7; Za 72:10-15
[f]**9:25** 1Sam 8:11; 1Fal 4:26; 10:26; 2Nya 1:14
[g]**9:26** 1Fal 2:21; Za 72:8-9; Mwa 15:18-21; 1Fal 4:21
[h]**9:27** 1Fal 10:27
[i]**9:28** Kum 17:16; 1Fal 10:26; Isa 31:1; 2:7; 2Nya 1:16
[j]**9:29** 2Sam 7:2; 1Nya 29:29; 1Fal 11:29; 2Nya 10:2; 12:15; 13:22
[k]**9:30** 1Fal 11:42-43
[l]**9:31** 1Fal 2:10
[m]**10:1** 1Fal 12:11
[n]**10:2** 1Fal 11:40; 2Nya 9:29
[o]**10:4** 2Nya 2:2; 1Sam 8:11-18; Mt 23:4; 1Fal 4:7; 5:15; 9:15; Mt 11:29-30; 1Yn 5:3
[p]**10:6** Ay 12:12; 32:7; 8:8-9
[q]**10:7** Mit 15:1; Neh 5:19; 1Fal 12:7; Za 112:5

wa watu hawa na kuwahudumia na kuwapa
jibu linaloridhisha, watakuwa watumishi
wako daima."
8 [a]Lakini Rehoboamu akakataa shauri
alilopewa na wazee na akataka ushauri
kwa vijana wanaume rika lake waliokuwa
wakimtumikia. 9 Akawauliza, "Ninyi
ushauri wenu ni nini? Tutawajibuje watu
hawa wanaoniambia, 'Ifanye nyepesi nira
baba yako aliyoweka juu yetu?' "
10 Wale vijana wa rika lake wakamjibu,
"Waambie watu hawa waliokuambia, 'Baba
yako aliweka nira nzito juu yetu, lakini
ifanye nira yetu nyepesi,' kuwa, 'Kidole
changu kidogo ni kinene kuliko kiuno cha
baba yangu. 11 Baba yangu aliweka nira
nzito juu yenu, mimi nitaifanya hata iwe
nzito zaidi. Baba yangu aliwachapa kwa
mijeledi; mimi nitawachapa kwa nge.' "
12 Siku tatu baadaye, Yeroboamu na
watu wote wakamrudia Rehoboamu, kama
mfalme alivyokuwa amesema, "Rudini
kwangu baada ya siku tatu." 13 [b]Mfalme
akawajibu watu kwa ukatili. Akikataa
shauri alilopewa na wazee, 14 akafuata
shauri la vijana wa rika lake na kusema,
"Baba yangu alifanya nira yenu kuwa
nzito, mimi nitaifanya kuwa nzito zaidi.
Baba yangu aliwachapa kwa mijeledi,
mimi nitawachapa kwa nge." 15 [c]Kwa hiyo
mfalme hakuwasikiliza watu, kwa kuwa
jambo hili lilitoka kwa Mungu ili kutimiza
neno ambalo BWANA alikuwa amenena kwa
Yeroboamu mwana wa Nebati kupitia Ahiya
Mshiloni.
16 [d]Israeli wote walipoona kuwa mfalme
amekataa kuwasikiliza, wakamjibu mfalme:

"Tuna fungu gani kwa Daudi?
Sisi hatuna urithi kwa mwana wa Yese.
Nendeni kwenye mahema yenu, ee Israeli,
angalia nyumba yako mwenyewe, ee Daudi!"

Hivyo Waisraeli wakaenda kwenye mahema
yao. 17 Lakini kwa habari ya Waisraeli
waliokuwa wakiishi katika miji ya Yuda,
Rehoboamu akaendelea kuwatawala bado.
18 [e]Mfalme Rehoboamu akamtuma
Adoniramu[f] aliyekuwa msimamizi wa wale
waliofanya kazi ngumu kwa kulazimishwa,
lakini Israeli wote wakampiga kwa mawe
hadi akafa. Hata hivyo, Mfalme Rehoboamu,
akafanikiwa kuingia kwenye gari lake na
kutorokea Yerusalemu. 19 [g]Hivyo Israeli
wakaasi dhidi ya nyumba ya Daudi hadi leo.

*Utabiri Wa Shamaya*

**(1 Wafalme 12:21-24)**

11 [h]Ikawa Rehoboamu alipofika
Yerusalemu, akakusanya nyumba ya
Yuda na ya Benyamini, wanaume wapiganaji
180,000, kufanya vita dhidi ya nyumba
ya Israeli na kuurudisha tena ufalme kwa
Rehoboamu mwana wa Solomoni.
2 [i]Lakini neno hili la BWANA likamjia
Shemaya mtu wa Mungu: 3 "Mwambie
Rehoboamu mwana wa Solomoni mfalme
wa Yuda, na Israeli wote walioko Yuda na
Benyamini, 4 [j]'Hili ndilo asemalo BWANA:
Msipande kupigana dhidi ya ndugu zenu.
Nendeni nyumbani, kila mmoja wenu, kwa
kuwa hili nimelitenda mimi.' " Kwa hiyo
wakalitii neno la BWANA na wakaacha
kwenda kupigana dhidi ya Yeroboamu.

*Yeroboamu Ajengea Yuda Ngome*

5 Rehoboamu akaishi Yerusalemu
akajenga miji yenye ngome katika Yuda:
6 [k]Akajenga Bethlehemu, Etamu, Tekoa,
7 Beth-Suri, Soko, Adulamu, 8 Gathi,
Maresha, Zifu, 9 Adoraimu, Lakishi, Azeka,
10 Sora, Aiyaloni na Hebroni. Hii ndiyo

[a]**10:8** 2Sam 17:14; Mit 13:20; 2Nya 25:16; Mit 1:25; Mhu 10:2
[b]**10:13** Mit 12:13; 14:16
[c]**10:15** Mwa 50:20; 2Nya 25:16-20; 11:4; 1Fal 11:29; Amo 3:6; 1Sam 2:25; 1Fal 12:15, 24
[d]**10:16** 1Nya 9:1; 2Sam 20:1
[e]**10:18** 2Sam 20:24; 1Fal 5:14
[f]18 Kiebrania ni Hadoramu.
[g]**10:19** 1Fal 12:19; 2Fal 17:21-23; 2Nya 13:5-7; Mhu 2:9
[h]**11:1** 1Fal 12:21
[i]**11:2** 1Sam 2:27; 1Fal 12:22-24; 2Nya 12:15; Kum 33:1; 2Nya 8:14; 1Tim 6:11
[j]**11:4** 2Nya 28:8-11; 28:8-11
[k]**11:6** Mwa 35:19; Amu 15:8; 1Sam 17:12; 2Nya 20:20; 2Sam 14:2; Neh 3:5; Yer 3:5; 6:1; Amo 1:1

iliyokuwa miji iliyojengewa ngome katika
Yuda na Benyamini. 11 Akaimarisha ulinzi
wake na kuweka majemadari ndani yake,
pamoja na ghala za mahitaji ya vyakula,
mafuta ya zeituni na divai. 12 Akaweka ngao
na mikuki katika miji na kuifanya iwe imara
sana. Kwa hiyo Yuda na Benyamini zikawa
zake.

13 Makuhani na Walawi kutoka sehemu
zote za Israeli wakawa upande wake. 14 [a]Pia
Walawi wakaacha maeneo yao ya malisho
na mali zao, wakaja Yuda na Yerusalemu
kwa sababu Yeroboamu na wanawe
walikuwa wamewakataa wasiwe makuhani
wa BWANA. 15 [b]Naye akawa amechagua
makuhani wake mwenyewe kwa ajili
ya mahali pa juu pa kuabudia sanamu
za mbuzi na za ndama ambazo alikuwa
ametengeneza. 16 [c]Wale waliotoka katika
kila kabila la Israeli ambao walielekeza
mioyo yao kumtafuta BWANA, Mungu
wa Israeli, wakawafuata Walawi huko
Yerusalemu kumtolea BWANA dhabihu,
Mungu wa baba zao. 17 [d]Wakaimarisha
ufalme wa Yuda na kumuunga mkono
Rehoboamu mwana wa Solomoni miaka
mitatu, wakienenda katika njia za Daudi
na Solomoni katika wakati huu.

*Jamaa Ya Rehoboamu*

18 Rehoboamu alimwoa Mahalati ambaye
alikuwa binti Yeremothi mwana wa Daudi,
mamaye alikuwa Abihaili binti Eliabu
mwana wa Yese. 19 [e]Mahalati alimzalia
Rehoboamu wana: Yeushi, Shemaria na
Zahamu. 20 [f]Kisha akamwoa Maaka binti
Absalomu, ambaye alimzalia: Abiya,
Atai, Ziza na Shelomithi. 21 [g]Rehoboamu
akampenda Maaka binti Absalomu zaidi
kuliko wakeze wengine na masuria wake.
Kwa jumla alikuwa na wake kumi na
wanane na masuria sitini, wana ishirini
na wanane na binti sitini.

22 [h]Rehoboamu akamweka Abiya
mwana wa Maaka, kuwa mkuu wa wana
wa mfalme miongoni mwa ndugu zake
ili amfanye mfalme. 23 [i]Akatenda kwa
busara, akiwasambaza baadhi ya wanawe
katika wilaya zote za Yuda na Benyamini,
pamoja na miji yote yenye ngome. Akawapa
mahitaji tele na kuwaoza wake wengi.

*Shishaki Ashambulia Yerusalemu*

**(1 Wafalme 14:25-28)**

12 [j]Baada ya nafasi ya Rehoboamu
kuimarika na kuwa na nguvu,
yeye na Israeli yote waliiacha sheria ya
BWANA Mungu. 2 [k]Kwa sababu hawakuwa
waaminifu kwa BWANA, Shishaki mfalme
wa Misri akashambulia Yerusalemu katika
mwaka wa tano wa utawala wa Mfalme
Rehoboamu. 3 [l]Akiwa na magari ya vita
1,200 na wapanda farasi 60,000 na idadi
isiyohesabika ya majeshi ya Walibia,
Wasukii na Wakushi[m] yaliyokuja pamoja
naye kutoka Misri. 4 [n]Akateka miji ya
Yuda yenye ngome akaendelea mpaka
Yerusalemu.

5 [o]Ndipo nabii Shemaya akaja kwa
Rehoboamu na kwa viongozi wa Yuda
waliokuwa wamekusanyika huko
Yerusalemu kwa ajili ya hofu ya Shishaki
naye akawaambia, "Hivi ndivyo asemavyo
BWANA, 'Ninyi mmeniacha mimi, kwa hiyo,
mimi nami sasa ninawaacha ninyi mkononi
mwa Shishaki.' "

6 [p]Viongozi wa Israeli na mfalme
wakajinyenyekeza na kusema, "BWANA
Mungu ni mwenye haki."

---

[a]**11:14** Hes 35:2-5; 1Nya 6:81; 2Nya 13:9; 1Fal 12:28-33
[b]**11:15** 1Fal 12:28-31; 13:33; Law 17:7; 2Nya 13:8; Kum 32:15-17; Hos 13:2; 1Kor 10:20; Ufu 16:14; 1Fal 12:28
[c]**11:16** 2Nya 15:9; Za 69:32; 2Nya 30:11
[d]**11:17** 2Nya 12:1; Mt 13:18; Hos 6:4
[e]**11:19** 1Fal 15:2
[f]**11:20** 1Fal 15:2; 2Nya 12:16
[g]**11:21** Kum 15:17
[h]**11:22** Kum 21:15-17
[i]**11:23** Kum 17:17; 1Fal 11:3
[j]**12:1** 2Nya 11:17; Kum 8:14; 1Fal 14:22-24
[k]**12:2** 1Nya 5:25; 1Fal 11:40; 14:24-25
[l]**12:3** Mwa 10:6; Amo 9:7; 2Nya 16:8
[m]3 Yaani watu kutoka sehemu ya Naili ya juu.
[n]**12:4** 2Nya 11:10
[o]**12:5** 2Nya 11:1; Kum 28:15; 2Nya 15:1-2
[p]**12:6** Law 26:40-42; Ezr 9:15; Yak 4:10; Kut 9:27; 10:3; 2Nya 33:12; 34:27; Za 78:34

7 [a]BWANA Mungu alipoona kwamba
wamejinyenyekeza, neno hili la
BWANA likamjia Shemaya: “Maadamu
wamejinyenyekeza, sitawaangamiza
bali hivi karibuni nitawapatia wokovu.
Ghadhabu yangu haitamwagwa juu ya
Yerusalemu kwa kupitia Shishaki. 8 [b]Hata
hivyo, watamtumikia Shishaki ili wapate
kujifunza tofauti kati ya kunitumikia
mimi na kuwatumikia wafalme wa nchi
nyingine.”
9 [c]Shishaki mfalme wa Misri
alipoishambulia Yerusalemu, alichukua
hazina za Hekalu la BWANA na hazina za
jumba la kifalme. Akachukua kila kitu,
pamoja na zile ngao za dhahabu ambazo
Solomoni alikuwa amezitengeneza. 10 [d]Kwa
hiyo Mfalme Rehoboamu akatengeneza
ngao za shaba badala ya zile za dhahabu na
kuzikabidhi kwa majemadari wa ulinzi wa
zamu kwenye ingilio la jumba la mfalme.
11 Kila wakati mfalme alipokwenda katika
Hekalu la BWANA walinzi walikwenda
pamoja naye wakiwa wamebeba hizo ngao
na baadaye walizirudisha kwenye chumba
cha ulinzi.
12 [e]Kwa sababu Rehoboamu
alijinyenyekeza, hasira ya BWANA
ikageukia mbali naye, hakuangamizwa
kabisa. Kukawa na hali nzuri katika Yuda.
13 [f]Mfalme Rehoboamu akajiweka
imara katika Yerusalemu na akaendelea
kuwa mfalme. Alikuwa na umri wa miaka
arobaini na mmoja alipoanza kutawala,
naye akatawala huko Yerusalemu miaka
kumi na saba, mji ambao BWANA alikuwa
ameuchagua miongoni mwa makabila yote
ya Israeli ili aliweke Jina lake humo. Mama
yake aliitwa Naama, alikuwa Mwamoni.
14 [g]Rehoboamu akatenda maovu kwa sababu
hakuuelekeza moyo wake katika kumtafuta
BWANA Mungu.
15 [h]Kwa habari ya matukio katika
utawala wa Rehoboamu, tangu mwanzo
mpaka mwisho, je, hayakuandikwa katika
kumbukumbu za nabii Shemaya na mwonaji
Ido zinazohusiana na vizazi? Kulikuwako
na vita mara kwa mara kati ya Rehoboamu
na Yeroboamu. 16 [i]Rehoboamu akalala na
baba zake, akazikwa katika Mji wa Daudi.
Naye Abiya mwanawe akawa mfalme baada
yake.

*Abiya Mfalme Wa Yuda*

**(1 Wafalme 15:1-8)**

13 Katika mwaka wa kumi na nane wa
utawala wa Yeroboamu, Abiya akawa
mfalme wa Yuda, 2 [j]naye akatawala huko
Yerusalemu miaka mitatu. Mama yake
aliitwa Maaka, binti Urieli wa Gibea.
Basi kulikuwa na vita kati ya Abiya na
Yeroboamu. 3 Abiya aliingia vitani na jeshi
la watu 400,000 wenye uwezo wa kupigana,
naye Yeroboamu akapanga jeshi dhidi ya
Abiya akiwa na jeshi la watu 800,000
wenye uwezo.
4 [k]Abiya akasimama juu ya Mlima
Semaraimu, katika nchi ya vilima ya
Efraimu, naye akasema, “Yeroboamu
na Israeli yote, nisikilizeni mimi!
5 [l]Hamfahamu kwamba BWANA, Mungu
wa Israeli, alimpa Daudi na wazao wake
ufalme juu ya Israeli milele kwa Agano la
chumvi? 6 [m]Hata hivyo Yeroboamu mwana
wa Nebati afisa wa Solomoni mwana wa
Daudi, aliasi dhidi ya bwana wake. 7 [n]Baadhi
ya watu wasiofaa kitu, wabaya kabisa
walimkusanyikia na kumpinga Rehoboamu
mwana wa Solomoni alipokuwa kijana
mdogo asiyekuwa na uamuzi, asiye na
nguvu za kuweza kupingana nao.

---

[a]**12:7** 1Fal 21:29; Za 78:38
[b]**12:8** Kum 28:48; Isa 26:13
[c]**12:9** 2Nya 9:16; 1Fal 14:25
[d]**12:10** 2Sam 8:18; 23:23; 1Nya 11:25
[e]**12:12** 1Fal 14:13; 2Nya 19:3; Mwa 18:24
[f]**12:13** 2Nya 6:6; 13:7; Kum 12:5; 1Fal 14:21; Za 48:1-3
[g]**12:14** Mt 7:7; Mdo 9:11
[h]**12:15** 2Nya 9:29; 13:22
[i]**12:16** 2Nya 11:20
[j]**13:2** 2Nya 11:20; 1Fal 15:6
[k]**13:4** Yos 18:22; 1Nya 11:1
[l]**13:5** 2Sam 7:13; 1Nya 17:12; Law 2:13; Hes 18:19; Amu 11:21-24; Eze 43:24; 1Sam 16:13; Za 89:20; Lk 1:31-33
[m]**13:6** 1Fal 11:26; 12:20; 2Nya 10:19
[n]**13:7** Amu 9:4; Za 26:4; Mdo 17:5; Mit 12:11

8 [a][b]“Hata sasa unapanga kupingana na ufalme wa BWANA ambao uko mikononi mwa wazao wa Daudi. Kweli ninyi ni jeshi kubwa nanyi mnazo ndama za dhahabu Yeroboamu alizozitengeneza kuwa miungu yenu. 9 [c]Lakini je, hamkuwafukuza makuhani wa BWANA, wana wa Aroni na Walawi na kujifanyia makuhani wenu wenyewe kama yafanyavyo mataifa ya nchi nyingine? Yeyote anayekuja kujiweka wakfu akiwa na ndama dume na kondoo dume saba aweza kuwa kuhani wa kile ambacho ni miungu kwenu.

10 “Lakini kwetu sisi, BWANA ndiye Mungu wetu, wala hatujamwacha. Makuhani wanaomtumikia BWANA ni wana wa Aroni, nao Walawi wakiwasaidia. 11 [d]Kila asubuhi na jioni wao hutoa sadaka za kuteketezwa na kufukiza uvumba wa harufu nzuri kwa BWANA. Wao huweka mikate juu ya meza safi kwa taratibu za kiibada na kuwasha taa kwenye kinara cha dhahabu kila jioni. Sisi tunazishika kanuni za BWANA Mungu wetu. Lakini ninyi mmemwacha Mungu. 12 [e]Mungu yu pamoja nasi, yeye ndiye kiongozi wetu. Makuhani wake wakiwa na tarumbeta zao watapiga baragumu ya vita dhidi yenu. Watu wa Israeli, msipigane dhidi ya BWANA, Mungu wa baba zenu, kwa maana hamtashinda.”

13 [f]Basi Yeroboamu alikuwa ametuma jeshi kuzunguka nyuma ya Yuda ili kwamba akiwa mbele ya Yuda, jeshi liwavizie kwa nyuma. 14 [g]Basi Yuda wakageuka na kuona kwamba wanashambuliwa mbele na nyuma. Ndipo wakamlilia BWANA. Makuhani wakapiga tarumbeta zao, 15 [h]nao watu wa Yuda wakapaza sauti ya kilio cha vita. Katika kupiga kelele za vita, Mungu akawafukuza Yeroboamu na Israeli wote mbele ya Mfalme Abiya na Yuda. 16 [i]Waisraeli wakakimbia mbele ya Yuda, naye Mungu akawatia Israeli mikononi mwao. 17 Abiya na watu wake wakawachinja kwa machinjo makuu, hata wakawepo majeruhi 500,000 miongoni mwa watu wenye uwezo wa Israeli. 18 [j]Watu wa Israeli walitiishwa katika tukio lile, nao watu wa Yuda wakawa washindi kwa sababu walimtegemea BWANA, Mungu wa baba zao.

19 [k]Abiya akamfuatia Yeroboamu na kuteka miji ya Betheli, Yeshana na Efroni kutoka kwake, pamoja na vijiji vinavyoizunguka miji hiyo. 20 [l]Yeroboamu hakupata nguvu tena wakati wa utawala wa Abiya. Naye BWANA akampiga Yeroboamu akafa.

21 Lakini Abiya akapata nguvu. Alioa wanawake kumi na wanne na alikuwa na wana ishirini na wawili na binti kumi na sita.

22 [m]Matukio mengine ya utawala wa Abiya, pamoja na mambo aliyofanya na aliyosema, yameandikwa katika kitabu cha maelezo cha nabii Ido.

### *Asa Atawala*

14 [n]Naye Abiya akalala na baba zake, akazikwa katika Mji wa Daudi. Asa mwanawe akawa mfalme baada yake. Katika siku zake, nchi ikawa na amani kwa miaka kumi.

2 Asa akatenda yaliyo mema na haki machoni pa BWANA Mungu wake. 3 [o]Akaziondoa madhabahu za kigeni na mahali pa juu pa kuabudia miungu, akayavunja yale mawe ya kuabudiwa na kuzikatakata nguzo za Maashera.

[a]**13:8** Za 68:25; 1Nya 25:10-24; 2Nya 29:25
[b]**13:8** Kut 32:4; 1Fal 12:28; Hos 8:6
[c]**13:9** 2Nya 11:14-15; Kut 29:35-36; Gal 4:8; Yer 2:11
[d]**13:11** Kut 29:39; 2Nya 2:4; Law 24:2-6; 1Nya 9:24; Kut 27:20-21
[e]**13:12** Hes 10:8-9; Amu 2:15; Mdo 5:39; Kum 20:4; Yos 5:4; Za 20:7; Ay 15:25-26; Mdo 9:4-5
[f]**13:13** 2Nya 20:22; Yos 8:9
[g]**13:14** 1Nya 5:20; 2Nya 18:31
[h]**13:15** 2Nya 14:12; Hes 32:4
[i]**13:16** 2Nya 16:8
[j]**13:18** 1Nya 5:20; Za 22:5; Amu 8:28; 2Fal 18:5; 2Nya 16:8-9; 20:20
[k]**13:19** Yos 15:9; Yn 11:54
[l]**13:20** 1Sam 25:38; Eze 24:16; Mdo 12:23; 1Sam 26:10; 1Fal 14:20
[m]**13:22** 2Nya 9:29; 12:15
[n]**14:1** 1Fal 15:8
[o]**14:3** Kum 7:5; 1Fal 15:12-14; Kut 34:13; 2Nya 15:17; 1Fal 11:7

4 Akawaamuru Yuda kumtafuta BWANA,
Mungu wa baba zao na kutii sheria zake
na amri zake. 5 [a]Akaondoa mahali pa juu
pa kuabudia miungu na madhabahu za
kufukizia uvumba kwenye kila mji katika
Yuda, nao ufalme ulikuwa na amani katika
utawala wake. 6 [b]Akajenga miji yenye
ngome katika Yuda, wakati nchi ikiwa na
amani. Hakuna mtu yeyote aliyepigana vita
naye katika miaka hiyo, kwa kuwa BWANA
alimstarehesha.
7 Mfalme akawaambia Yuda, "Tuijenge
hii miji na tuizungushie kuta, pamoja na
minara, malango na makomeo. Nchi bado
ni yetu, kwa sababu tumemtafuta BWANA
Mungu wetu, tulimtafuta naye ametupa
raha kila upande." Hivyo wakajenga na
wakafanikiwa.
8 Asa alikuwa na jeshi la watu 300,000
kutoka Yuda, wenye ngao kubwa na mikuki
na jeshi la watu 280,000 kutoka Benyamini,
wenye ngao ndogo na pinde. Watu hawa
wote walikuwa wapiganaji mashujaa.
9 [c]Zera Mkushi akatoka kupigana dhidi
yao akiwa na jeshi la watu maelfu ya maelfu
na magari ya vita 300, nao wakaja mpaka
Maresha. 10 Asa akatoka kumkabili, nao
wakapanga vita katika Bonde la Sefatha
karibu na Maresha.
11 [d]Kisha Asa akamlilia BWANA Mungu
wake na kusema, "Ee BWANA, hakuna
yeyote aliye kama wewe wa kuwasaidia
wasio na nguvu dhidi ya wenye nguvu.
Utusaidie, Ee BWANA, wewe ndiwe Mungu
wetu, kwa kuwa tunakutumainia wewe,
nasi kwa jina lako tumekuja dhidi ya jeshi
hili kubwa. Ee BWANA, wewe ndiwe Mungu
wetu, usiwaache wanadamu wakushinde
wewe."
12 [e]BWANA akawapiga Wakushi mbele
ya Asa na Yuda. Wakushi wakakimbia,
13 [f]naye Asa na jeshi lake wakawafuatia
mpaka Gerari. Idadi kubwa ya Wakushi
ilianguka hata wasiweze kuinuka tena,
wakapondapondwa mbele za BWANA na
majeshi yake. 14 [g]Watu wa Yuda wakachukua
nyara nyingi sana, wakaangamiza vijiji
vyote vinavyoizunguka Gerari, kwa kuwa
hofu ya BWANA ilikuwa imewaangukia.
Wakateka nyara vijiji hivi vyote, kwani
kulikuwepo nyara nyingi huko. 15 Pia
wakashambulia kambi za wachunga
makundi ya wanyama wakachukua na
kuyaswaga makundi ya kondoo, mbuzi na
ngamia. Kisha wakarudi Yerusalemu.

*Asa Afanya Matengenezo*

15 [h]Roho wa BWANA akamjia Azaria
mwana wa Odedi. 2 [i]Akatoka ili
kumlaki Asa na kumwambia, "Nisikilizeni,
Asa na Yuda wote na Benyamini. BWANA yu
pamoja nanyi mkiwa pamoja naye. Kama
mkimtafuta, ataonekana kwenu, lakini
kama mkimwacha yeye, naye atawaacha
ninyi. 3 [j]Kwa muda mrefu Israeli walikuwa
hawana Mungu wa kweli, walikuwa
hawana kuhani wa kuwafundisha na wala
hawakuwa na sheria. 4 [k]Lakini katika taabu
yao walimrudia BWANA, Mungu wa Israeli
na kumtafuta, naye akaonekana kwao.
5 [l]Katika siku hizo hapakuwa na amani
kwa yeyote aliyesafiri, kutoka wala kuingia,
kwa kuwa wakazi wote wa nchi walikuwa
katika machafuko makubwa. 6 [m]Taifa moja
lilipigana na taifa lingine na mji mmoja
ukapigana na mji mwingine, kwa sababu
Mungu alikuwa anawahangaisha kwa
taabu za kila aina. 7 [n]Lakini kwa habari

[a]**14:5** Isa 27:9; Eze 6:4
[b]**14:6** 1Nya 22:9; 2Nya 15:15
[c]**14:9** 2Nya 16:8; 12:3; Yos 15:44; Mwa 10:8-9; Mik 1:15
[d]**14:11** 1Fal 8:44, 45; 2Nya 25:8; 13:18; Kut 14:10; 1Sam 14:6; 17:45; 1Nya 5:20; Za 22:5; Mdo 2:21; Amu 7:7; 2Kor 12:9-10; Mit 18:10; Nah 1:7
[e]**14:12** 2Nya 13:15
[f]**14:13** Mwa 10:19; Za 46:1-11
[g]**14:14** Mwa 35:5; Kum 2:25; 11:25; Kut 15:16; 2Nya 17:10; 20:29
[h]**15:1** Hes 24:4; Amu 3:10; 2Nya 24:20; 2Sam 23:2; 2Nya 20:14; 2Pet 1:21
[i]**15:2** Yak 4:8; 2Nya 20:17; Kum 31:17; 1Nya 28:9; Ebr 12:25; 2Nya 33:12-13; Yer 29:13; Mt 7:7; 2Nya 12:1-3; Rum 11:1-2
[j]**15:3** Law 10:11; Mao 2:9; Amo 8:11; Hos 3:4
[k]**15:4** Kum 4:29
[l]**15:5** Amu 19:20; Zek 8:10; Amu 5:6
[m]**15:6** Mt 24:7; Isa 19:2; Mk 13:8
[n]**15:7** 1Sam 24:19; Mit 14:14; Rut 2:12; Za 58:11; Mt 5:12-46; Lk 6:35; Kol 3:24

yenu ninyi, kuweni hodari wala msikate tamaa, kwa kuwa mtapata thawabu kwa kazi yenu.”

8 [a]Asa aliposikia maneno haya na unabii wa Azaria mwana wa Odedi nabii, akajipa moyo. Akaziondoa sanamu zote zilizokuwa machukizo katika nchi yote ya Yuda na Benyamini na kutoka miji aliyoiteka ya vilima vya Efraimu. Akakarabati madhabahu ya Bwana iliyokuwa mbele ya ukumbi wa Hekalu la Bwana.

9 [b]Kisha akakutanisha Yuda wote, Benyamini na watu kutoka Efraimu, watu wa Manase na Simeoni waliokuwa wanaishi miongoni mwao, kwa maana idadi kubwa walikuwa wamemjia kutoka Israeli walipoona kwamba Bwana Mungu wake alikuwa pamoja naye.

10 Basi wakakusanyika huko Yerusalemu mwezi wa tatu katika mwaka wa kumi na tano wa utawala wa Asa. 11 [c]Wakati huo wakamtolea Bwana dhabihu za ng’ombe 700, kondoo na mbuzi 7,000 kutoka zile nyara walizoteka. 12 [d]Wakafanya agano kumtafuta Bwana, Mungu wa baba zao kwa moyo wao wote na kwa roho yao yote. 13 [e]Wale wote ambao hawangemtafuta Bwana, Mungu wa Israeli wangelazimika kuuawa, akiwa mdogo au mkubwa, mwanaume au mwanamke. 14 Wakamwapia Bwana kwa sauti kuu, kwa kupiga kelele, tarumbeta na kwa mabaragumu. 15 [f]Yuda wote wakafurahia kile kiapo kwa sababu walikuwa wameapa kwa moyo wao wote. Wakamtafuta Mungu kwa bidii, naye akaonekana kwao. Kwa hiyo Bwana akawastarehesha pande zote.

16 [g]Mfalme Asa akamwondolea Maaka mama yake wadhifa wake kama mama malkia kwa sababu alikuwa ametengeneza nguzo ya Ashera ya kuchukiza. Asa akaikata hiyo nguzo, akaivunjavunja na kuiteketeza kwa moto katika Bonde la Kidroni. 17 [h]Ijapokuwa hakuondoa mahali pa juu pa kuabudia miungu katika Israeli, moyo wa Asa ulikuwa umejiweka kwa Bwana kikamilifu maisha yake yote. 18 Akaleta ndani ya Hekalu la Mungu fedha na dhahabu na vile vyombo ambavyo yeye na baba yake walikuwa wameviweka wakfu.

19 Hapakuwepo vita tena mpaka mwaka wa thelathini na tano wa utawala wake Asa.

*Miaka Ya Mwisho Ya Mfalme Asa*

**(1 Wafalme 15:17-24)**

16 [i]Katika mwaka wa thelathini na sita wa utawala wa Asa, Mfalme Baasha wa Israeli akashambulia Yuda na kuweka ngome mji wa Rama ili kumzuia yeyote asitoke wala kuingia nchi ya Mfalme Asa wa Yuda.

2 Ndipo Asa akachukua fedha na dhahabu kutoka hazina ya Hekalu la Bwana na kutoka jumba lake mwenyewe la kifalme na kumpelekea Ben-Hadadi mfalme wa Aramu, ambaye alikuwa anatawala huko Dameski. 3 [j]Akasema, “Pawepo na mkataba kati yangu na wewe, kama ulivyokuwepo kati ya baba yangu na baba yako. Tazama, nimekuletea fedha na dhahabu. Sasa vunja mkataba wako na Baasha mfalme wa Israeli ili aniondokee mimi.”

4 Ben-Hadadi akakubaliana na Mfalme Asa na kutuma majemadari wa majeshi yake dhidi ya miji ya Israeli. Wakashinda Iyoni, Dani, Abel-Maimu na miji yote ya hazina ya Naftali. 5 Baasha aliposikia jambo hili, akasimamisha kujenga Rama na kuacha kazi yake. 6 Ndipo Mfalme Asa akawaleta watu wote wa Yuda, nao wakachukua mawe na miti ambayo Baasha alikuwa anavitumia huko Rama. Kwa vitu hivyo akajenga Geba na Mispa.

7 [k]Ikawa wakati huo mwonaji Hanani akamjia Mfalme Asa wa Yuda na kumwambia: “Kwa sababu ulimtegemea

[a]**15:8** 2Nya 13:19; 8:12; 1Fal 8:64
[b]**15:9** 2Nya 11:16-17
[c]**15:11** 2Nya 14:13-15
[d]**15:12** 2Fal 11:17; 2Nya 23:16; Neh 10:29; 1Nya 16:11; 2Fal 23:3; 2Nya 34:31
[e]**15:13** Kut 22:20; Kum 13:9-16
[f]**15:15** Kum 4:29; 1Nya 22:9; 2Nya 14:7
[g]**15:16** Kut 34:13; 2Nya 14:2-5; 1Fal 15:2, 10
[h]**15:17** 2Fal 12:3; 1Fal 3:2-4; Kum 12:7; 1Fal 15:14; 2Nya 14:3-5
[i]**16:1** Yer 41:9; 2Nya 15:9; 1Fal 15:17
[j]**16:3** 2Nya 20:35; 25:7
[k]**16:7** 1Fal 16:1; 2Nya 19:2; 20:34; Za 146:3-6; Isa 31:1; Yer 17:5

mfalme wa Aramu nawe hukumtegemea
BWANA Mungu wako, jeshi la mfalme wa
Aramu limeponyoka mkononi mwako. 8 [a]Je,
hukumbuki lililotendeka kwa Wakushi na
Walibia, hawakuwa jeshi lenye nguvu na
magari mengi ya vita na wapanda farasi?
Hata hivyo, ulipomtegemea BWANA
yeye aliwatia mkononi mwako. 9 [b]Kwa
kuwa macho ya BWANA hukimbiakimbia
duniani kote ili kujionyesha mwenye
nguvu kwa ajili ya wale ambao mioyo yao
inamtegemea kwa ukamilifu. Umefanya
jambo la upumbavu na kuanzia sasa na
kuendelea utakuwa na vita."
10 [c]Asa akamkasirikia mwonaji kwa sababu
ya jambo hili. Alikuwa ameghadhibika sana
hata akamweka gerezani. Wakati huo huo
Asa akaanza kuwatesa na kuwaonea baadhi
ya watu kwa ukatili.
11 Matukio ya utawala wa Asa, kuanzia
mwanzo mpaka mwisho, yameandikwa
katika kitabu cha wafalme wa Yuda na
Israeli. 12 [d]Katika mwaka wa thelathini
na tisa wa utawala wake, Asa alipatwa
na ugonjwa kwenye miguu yake. Ingawa
ugonjwa wake ulimzidia sana, hata katika
kuugua kwake hakutafuta msaada kutoka
kwa BWANA bali kwa matabibu tu. 13 Katika
mwaka wa arobaini na moja wa utawala wa
Asa, alikufa na kulala na baba zake. 14 [e]Nao
wakamzika katika kaburi lile alilokuwa
amejichongea mwenyewe katika Mji wa
Daudi. Wakamzika kwa jeneza lililowekwa
vikolezi na mchanganyiko wa manukato
ya aina mbalimbali yaliyotengenezwa kwa
utaalamu wa mtengeneza marashi, nao
wakawasha moto mkubwa kwa heshima
yake.

[a]**16:8** Mwa 10:6-9; 2Nya 13:16; 14:9; 12:3
[b]**16:9** Ay 24:23; 1Sam 13:13; Za 33:13-15; Yer 5:21; 32:19; 1Kor 15:36; 2Nya 6:20; Ay 34:21; Yer 16:17; Zek 4:10; Ebr 4:13; 1Pet 3:12; 1Nya 21:8; Mt 5:22; 1Fal 15:32
[c]**16:10** 2Nya 18:26; Yer 20:2; Mt 14:3
[d]**16:12** Yer 17:5-6; Kum 28:22
[e]**16:14** Mwa 50:2; Yn 19:39-40; Mk 16:1; 2Nya 21:19; Yer 34:5

### *Yehoshafati Mfalme Wa Yuda*

17 Yehoshafati mwanawe akawa mfalme
baada yake na akajiimarisha dhidi ya
Israeli. 2 [f]Akaweka jeshi katika miji yote
ya Yuda yenye ngome na kuweka askari
walinzi katika Yuda na katika miji ya
Efraimu ile ambayo baba yake Asa alikuwa
ameiteka.
3 [g]BWANA Mungu alikuwa na Yehoshafati
kwa sababu katika miaka yake ya mwanzoni
alienenda katika njia za Daudi baba yake.
Hakutafuta Mabaali 4 [h]bali alimtafuta
Mungu wa baba yake na kuzifuata amri
zake badala ya kufuata desturi za watu wa
Israeli. 5 [i]Kwa hiyo BWANA akauimarisha
ufalme chini ya uongozi wake, nao Yuda
wote wakamletea Yehoshafati zawadi,
hivyo akawa na utajiri mwingi na heshima.
6 [j]Moyo wake ukawa hodari katika njia za
BWANA na zaidi ya yote, akaondoa mahali
pa juu pa kuabudia miungu na nguzo za
Maashera katika Yuda.
7 [k]Katika mwaka wa tatu wa utawala
wa akatuma maafisa wake ambao ni:
Ben-Haili, Obadia, Zekaria, Nethaneli
na Mikaya ili kufundisha katika miji ya
Yuda. 8 [l]Pamoja nao walikuwepo Walawi
fulani nao ni: Shemaya, Nethania, Zebadia,
Asaheli, Shemiramothi, Yehonathani,
Adoniya, Tobia, Tob-Adonia, pamoja
nao walikuwepo makuhani Elishama na
Yehoramu. 9 [m]Wakafundisha Yuda yote,
wakiwa wamechukua Kitabu cha Sheria ya
BWANA wakazunguka miji yote ya Yuda na
kufundisha watu.
10 [n]Hofu ya BWANA ikawa juu ya falme
zote za nchi zilizozunguka Yuda, hivyo
hawakufanya vita na Yehoshafati. 11 [o]Baadhi
ya Wafilisti wakamletea Yehoshafati zawadi

[f]**17:2** 2Nya 15:8; 11:11
[g]**17:3** Rum 8:31; 1Fal 22:43
[h]**17:4** 1Fal 12:28; 2Nya 22:9
[i]**17:5** 1Sam 10:27; 2Nya 18:1; 1Fal 10:25-27
[j]**17:6** 1Fal 8:61; 2Nya 14:3; 15:17
[k]**17:7** Neh 8:7; Mal 2:7; 2Nya 15:3
[l]**17:8** Hos 4:6
[m]**17:9** Kum 6:4-9; 28:61; Law 10:11; 2Nya 35:3; Neh 8:7; Mal 2:7
[n]**17:10** Mwa 35:5; Kum 2:25; Kut 15:15; 2Nya 14:14
[o]**17:11** 2Nya 9:14; 26:8; 21:16; 2Sam 8:2

na fedha kama ushuru, nao Waarabu
wakamletea mifugo: kondoo dume 7,700
na mbuzi 7,700.
12 Yehoshafati akaendelea kupata nguvu
zaidi na zaidi, akajenga ngome na miji ya
hazina katika Yuda 13 na akawa na wingi
mkubwa wa vitu katika miji ya Yuda. Pia
aliweka askari wa vita wenye uzoefu huko
Yerusalemu. 14 [a]Wakaandikishwa katika
jamaa zao kama ifuatavyo:

Kutoka Yuda, majemadari wa vikosi
vya elfu:
Jemadari Adna akiwa na askari wa
vita 300,000;
15 aliyefuata ni jemadari Yehohanani,
akiwa na askari 280,000 walio
tayari kwa vita;
16 [b]aliyefuata ni Amasia mwana
wa Zikri, ambaye alijitolea kwa
ajili ya kazi ya Bwana, akiwa na
askari 200,000.
17 Kutoka Benyamini:
Eliada, askari shujaa akiwa na
watu 200,000 wenye silaha za
nyuta na ngao;
18 aliyefuata ni Yehozabadi, akiwa
na askari 180,000 wenye silaha za
vita.

19 [c]Hawa ndio waliomtumikia mfalme,
mbali na wale mfalme aliweka katika miji
yenye ngome huko Yuda yote.

*Mikaya Atoa Unabii Dhidi Ya Ahabu*

**(1 Wafalme 22:1-28)**

18 [d]Basi, Yehoshafati alikuwa na mali
nyingi sana na heshima. Naye akafanya
urafiki na Ahabu kwa mwanawe kumwoa
binti wa Ahabu. 2 [e]Baada ya miaka kadhaa
akashuka kumtembelea Ahabu huko
Samaria. Ahabu akachinja ng'ombe na
kondoo wengi kwa ajili yake na watu
aliokuwa amefuatana nao. Kisha Ahabu
akamshawishi Yehoshafati kukwea pamoja
naye ili kuishambulia Ramoth-Gileadi.
3 Ahabu mfalme wa Israeli akamuuliza
Yehoshafati mfalme wa Yuda, "Je,
utakwenda pamoja nami kupigana dhidi
ya Ramoth-Gileadi?"

Yehoshafati akamjibu mfalme wa Israeli,
"Mimi ni kama wewe, watu wangu ni kama
watu wako, farasi wangu ni kama farasi
wako. Tutakuwa pamoja nawe vitani."
4 [f]Lakini Yehoshafati pia akamwambia
mfalme wa Israeli, "Kwanza tafuta shauri
la Bwana."
5 [g]Kwa hiyo mfalme wa Israeli akawaleta
pamoja manabii wanaume wapatao mia
nne, akawauliza, "Je, twende vitani dhidi
ya Ramoth-Gileadi, au niache?"

Wakajibu, "Naam, nenda kwa kuwa
Mungu ataiweka Ramoth-Gileadi mkononi
mwa mfalme."
6 Lakini Yehoshafati akauliza, "Je, hayuko
nabii wa Bwana hapa ambaye tunaweza
kumuuliza?"
7 Mfalme wa Israeli akamjibu Yehoshafati,
"Bado yupo mtu mmoja ambaye kupitia
yeye twaweza kumuuliza shauri la Bwana,
lakini namchukia kwa sababu huwa hatabiri
jambo lolote jema kunihusu mimi, lakini
kila mara hunitabiria mabaya tu. Yeye ni
Mikaya mwana wa Imla."

Yehoshafati akajibu, "Mfalme hapaswi
kusema hivyo."
8 Kwa hiyo mfalme wa Israeli akamwita
mmoja wa maafisa wake na kusema, "Mlete
Mikaya mwana wa Imla mara moja."
9 Wakiwa wamevalia majoho yao ya
kifalme, mfalme wa Israeli na Yehoshafati
mfalme wa Yuda walikuwa wameketi juu
ya viti vyao vya kifalme katika sakafu ya
kupuria, kwenye ingilio la lango la Samaria,
pamoja na manabii wote wakiwa wakitabiri
mbele yao. 10 Wakati huu Sedekia mwana
wa Kenaana alikuwa ametengeneza pembe
za chuma, akatangaza, "Hivi ndivyo Bwana
asemavyo, 'Kwa hizi pembe utawapiga na

[a]**17:14** 2Sam 24:2
[b]**17:16** Amu 5:9; 1Nya 29:9-17; 2Kor 8:12; Za 110:3
[c]**17:19** 2Nya 25:5; 11:10
[d]**18:1** 2Nya 17:5; 19:1-3; 21:6; Mhu 5:19; Mit 4:5-8; Za 112:2-9; Kum 8:10, 18; 1Sam 2:7, 30; 1Fal 3:13; 1Tim 4:8; 2Fal 8:18; 2Kor 6:14
[e]**18:2** 1Fal 22:2; 2Nya 19:2
[f]**18:4** 1Sam 23:2-9; Yer 21:2; Eze 20:3; 1Fal 22:5-6; 2Nya 34:26
[g]**18:5** Yer 23:17; Eze 13:3; Mt 23:16-19

kuwarudisha Waaramu nyuma mpaka
wameangamizwa.’ ”
11 [a]Manabii wengine wote walikuwa
wanatabiri kitu hicho hicho, wakisema,
“Ishambulie Ramoth-Gileadi na uwe
mshindi. Kwa kuwa BWANA ataitia mkononi
mwa mfalme.”
12 Mjumbe aliyekuwa amekwenda
kumwita Mikaya akamwambia, “Tazama,
manabii wote kama mtu mmoja wanatabiri
ushindi kwa mfalme. Neno lako na
likubaliane na lao, nawe unene mema
kuhusu mfalme.”
13 [b]Lakini Mikaya akasema, “Hakika
kama BWANA aishivyo, nitamwambia kile
tu BWANA atakachoniambia.”
14 [c]Alipofika, mfalme akamuuliza,
“Mikaya, je, twende vitani dhidi ya Ramoth-
Gileadi au niache?”
Akamjibu, “Shambulia na ushinde, kwa
kuwa watatiwa mkononi mwako.”
15 Mfalme akamwambia, “Je, ni mara
ngapi nitakuapisha ili usiniambie kitu
chochote ila kweli tu kwa jina la BWANA?”
16 [d]Ndipo Mikaya akajibu, “Niliona Israeli
wote wametawanyika vilimani kama
kondoo wasio na mchungaji, naye BWANA
akasema, ‘Watu hawa hawana bwana.
Mwache kila mmoja aende nyumbani kwa
amani.’ ”
17 Mfalme wa Israeli akamwambia
Yehoshafati, “Sikukuambia kwamba huwa
hatabiri jambo lolote jema kunihusu bali
mabaya tu?”
18 [e]Mikaya akaendelea, “Kwa hiyo lisikie
neno la BWANA: Nilimwona BWANA ameketi
juu ya kiti chake cha enzi pamoja na jeshi
lote la mbinguni likiwa limesimama upande
wa kulia na wa kushoto.
19 Naye BWANA
akasema, ‘Ni nani atakayemshawishi
Ahabu, mfalme wa Israeli, ili aishambulie
Ramoth-Gileadi na kukiendea kifo chake
huko?’
“Mmoja akapendekeza hili na mwingine
lile.
20 [f]Mwishoni, roho akajitokeza,
akasimama mbele za BWANA na kusema,
‘Nitamshawishi.’
“BWANA akauliza, ‘Kwa njia gani?’
21 [g]“Akasema, ‘Nitakwenda na kuwa roho
ya uongo katika vinywa vya manabii wake
wote.’
“BWANA akasema, ‘Utafanikiwa katika
kumshawishi. Nenda ukafanye hivyo.’
22 [h]“Kwa hiyo sasa BWANA ameweka roho
ya kudanganya ndani ya vinywa vya hawa
manabii wako wote. BWANA ameamuru
maafa kwa ajili yako.”
23 [i]Kisha Sedekia mwana wa Kenaana
akatoka na kumpiga Mikaya kofi usoni.
Akauliza, “Huyo Roho kutoka kwa BWANA
alipita njia gani alipotoka kwangu ili
kusema nawe?”
24 Mikaya akajibu, “Utagundua siku hiyo
utakapokwenda kujificha kwenye chumba
cha ndani.”
25 Kisha mfalme wa Israeli akaagiza,
“Mchukueni na mkamrudishe kwa Amoni
mtawala wa mji na kwa Yoashi mwana
wa mfalme.
26 [j]Mkaseme, ‘Hivi ndivyo
asemavyo mfalme: Mwekeni mtu huyu
gerezani na asipewe chochote ila mkate
na maji mpaka nitakaporudi salama.’ ”
27 Mikaya akasema, “Kama utarudi
salama, basi BWANA hajanena kupitia
kwangu.” Kisha akaongeza kusema,
“Zingatieni maneno yangu, enyi watu
wote!”

### *Ahabu Anauawa Huko Ramoth-Gileadi*

**(1 Wafalme 22:29-35)**

28 Basi mfalme wa Israeli na Yehoshafati
mfalme wa Yuda wakaenda Ramoth-
Gileadi.
29 [k]Mfalme wa Israeli akamwambia
Yehoshafati, “Nitaingia vitani nikiwa

[a]**18:11** 2Nya 22:5
[b]**18:13** Hes 22:18-20, 35; 1Fal 22:14; Mdo 20:27; Hes 23:12, 26; 24:13; Yer 23:8; 42:4; Eze 2:7; Mik 2:6-7; 1Kor 11:23; 1The 2:4
[c]**18:14** 1Fal 18:27; Amo 4:4
[d]**18:16** Hes 27:17; Eze 34:5-8
[e]**18:18** Dan 7:9; Za 103:20
[f]**18:20** Ay 1:6; 2The 2:9
[g]**18:21** Zek 13:2; Yn 8:44; Hos 4:12; 1Fal 22:21-22
[h]**18:22** Ay 12:16; Isa 19:14; Mt 24:24-25; 2The 2:9-11; Eze 14:9; Yak 1:13
[i]**18:23** Yer 20:2; Mk 14:65; Mdo 23:2
[j]**18:26** 1Sam 25:21; 2Nya 16:10; Ebr 11:36; Lk 23:2
[k]**18:29** 1Sam 28:8; Mit 10:24

nimejibadilisha, lakini wewe uvae majoho yako ya kifalme." Kwa hiyo mfalme wa Israeli akajibadilisha na kwenda vitani.

30 Wakati huu, mfalme wa Aramu alikuwa amewaagiza majemadari thelathini na wawili wa magari ya vita, "Msipigane na yeyote, mdogo au mkubwa, isipokuwa mfalme wa Israeli." 31 [a]Wakati wale majemadari wa magari ya vita walipomwona Yehoshafati, wakafikiri, "Hakika huyu ndiye mfalme wa Israeli." Kwa hiyo wakageuka ili wamshambulie, lakini Yehoshafati akapiga kelele, naye BWANA akamsaidia. Mungu akawaondoa kwake, 32 wale majemadari wakaona kwamba hakuwa mfalme wa Israeli nao wakaacha kumfuatilia.

33 Lakini mtu fulani akavuta upinde pasipo lengo na kumpiga mfalme wa Israeli katikati ya kiungio cha mavazi yake ya chuma, mfalme akamwambia mwendesha gari lake, "Geuza gari na uniondoe mimi katika mapigano, nimejeruhiwa." 34 [b]Vita vikaendelea mchana kutwa, naye mfalme wa Israeli akajitegemeza ndani ya gari lake kuwaelekea Waaramu hadi jioni. Basi jioni yake akafa.

### *Yehu Amkemea Yehoshafati*

19 Mfalme Yehoshafati wa Yuda akarudi salama kwenye jumba lake la kifalme huko Yerusalemu. 2 [c]Yehu mwonaji, mwana wa Hanani, akapanda kwenda kuonana naye akamwambia Mfalme Yehoshafati, "Je, utawasaidia waovu na kuwapenda wale wanaomchukia BWANA? Kwa sababu ya jambo hili, ghadhabu ya BWANA iko juu yako. 3 [d]Hata hivyo, kuna mema yaliyoonekana kwako, kwa kuwa umeondoa katika nchi nguzo za Ashera na umeukaza moyo wako katika kumtafuta Mungu."

### *Yehoshafati Aweka Waamuzi*

4 Yehoshafati aliishi huko Yerusalemu, naye akatoka akaenda tena miongoni mwa watu, kuanzia Beer-Sheba hadi nchi ya vilima ya Efraimu na kuwageuza wakamrudia BWANA, Mungu wa baba zao. 5 [e]Akawaweka waamuzi katika nchi, kwenye miji yote ya Yuda yenye maboma. 6 [f]Akawaambia, "Angalieni kwa makini yale mtendayo, kwa kuwa hamkuhukumu kwa ajili ya mwanadamu bali kwa ajili ya BWANA ambaye yu pamoja nanyi kila mtoapo hukumu. 7 [g]Basi sasa hofu ya BWANA na iwe juu yenu. Hukumuni kwa uangalifu, kwa kuwa kwa BWANA Mungu wetu hakuna jambo lisilo la haki, upendeleo, wala rushwa."

8 [h]Pia huko Yerusalemu, Yehoshafati akaweka baadhi ya Walawi, makuhani na viongozi wa jamaa za Waisraeli ili kutoa hukumu kwa ajili ya BWANA na kuamua magomvi. Nao waliishi huko Yerusalemu. 9 [i]Akawapa maagizo haya: "Ni lazima mtumike kwa uaminifu na kwa moyo wote katika kicho cha BWANA. 10 [j]Katika kila shauri lifikalo mbele yenu kutoka kwa ndugu zenu wale waishio katika miji, ikiwa ni la umwagaji wa damu au mambo mengine yahusuyo sheria, amri, hukumu au maagizo, inawapasa ninyi kuwaonya kwamba wasiingie katika hatia dhidi ya BWANA, la sivyo ghadhabu yake itakuja juu yenu na ndugu zenu. Tendeni hivyo, nanyi hamtatenda dhambi.

11 [k]"Amaria kuhani mkuu atakuwa juu yenu katika jambo lolote linalomhusu BWANA naye Zebadia mwana wa Ishmaeli, kiongozi wa kabila la Yuda, atakuwa juu yenu kwa jambo lolote linalomhusu mfalme, nao Walawi watatumika kama

---

[a]**18:31** 2Nya 13:14; Mit 13:20; Za 46:1
[b]**18:34** 2Nya 22:5
[c]**19:2** 1Fal 14:13; 16:1; 2Nya 12:12; 16:2-9; Ezr 7:10; 1Sam 9:9; Za 7:11; 2Nya 24:18; 32:25
[d]**19:3** 1Fal 16:1; 2Nya 16:2-9; 32:25; Mit 7:11; Za 139:21-22
[e]**19:5** Mwa 47:6; Kut 16:18; 18:26
[f]**19:6** Law 19:15; Kum 16:18-20; Mhu 5:8; Kum 1:7; 1:17; Za 82:1
[g]**19:7** Kum 32:4; Ay 8:3; Kut 18:16; Rum 2:11; 9:14; Mdo 10:34; Kum 10:17; Ay 34:19; Gal 2:6; Efe 6:9; 1Pet 1:17
[h]**19:8** 2Nya 17:8-13; 2Sam 23:3; Kum 16:18; 17:9-13; 1Nya 23:4; 26:19
[i]**19:9** 2Sam 23:3
[j]**19:10** Kum 17:8; Hes 16:46; Eze 3:18
[k]**19:11** 1Nya 28:20

maafisa mbele yenu. Tendeni kwa ujasiri,
naye BWANA atakuwa pamoja na wale
watendao vyema.”

20 [a]Ikawa baada ya jambo hili, Wamoabu
na Waamoni, pamoja na baadhi ya
Wameuni wakaja ili wapigane vita na
Yehoshafati.

2 [b]Watu fulani wakaja wakamwambia
Yehoshafati, “Jeshi kubwa linakuja dhidi
yako kutoka Edomu tokea ng’ambo ile
nyingine ya Bahari.[c] Tayari liko Hasason-
Tamari” (yaani En-Gedi). 3 [d]Yehoshafati
akaogopa, akaazimu kumtafuta BWANA, na
akatangaza kwa Yuda wote kufunga. 4 [e]Watu
wa Yuda wakakusanyika pamoja ili kutafuta
msaada kutoka kwa BWANA. Wakaja kutoka
kila mji wa Yuda ili kumtafuta.

5 Kisha Yehoshafati akasimama katika
kusanyiko la Yuda na Yerusalemu katika
Hekalu la BWANA, mbele ya ua mpya,
6 [f]akasema:

> “Ee BWANA, Mungu wa baba zetu, si
> wewe ndiwe uliye Mungu mbinguni?
> Si wewe ndiwe utawalaye juu ya falme
> zote za mataifa? Uweza na nguvu viko
> mkononi mwako, wala hakuna yeyote
> awezaye kushindana nawe. 7 [g]Je, si
> wewe, Ee Mungu wetu, uliyewafukuza
> wenyeji wa nchi hii mbele ya watu
> wako Israeli, ukawapa wazao wa
> Abrahamu, rafiki yako, hata milele?
> 8 [h]Wameishi ndani yake na humo
> wamekujengea mahali patakatifu kwa
> ajili ya Jina lako, wakisema: 9 [i]‘Kama
> maafa yakitujia, ikiwa ni upanga,
> hukumu, tauni, au njaa, tutasimama
> mbele zako, mbele ya Hekalu hili
> ambalo limeitwa kwa Jina lako na
> kukulilia katika shida yetu, nawe
> utatusikia na kutuokoa.’
>
> 10 [j]“Lakini sasa hawa watu wa
> kutoka Amoni, Moabu na Mlima
> Seiri, ambao hukuwaruhusu Israeli
> wazivamie nchi zao wakati walitoka
> Misri, hivyo wakageukia mbali nao na
> hawakuwaangamiza, 11 [k]tazama jinsi
> wanavyotulipa kwa kuja kututupa
> nje ya milki uliyotupa sisi kuwa
> urithi. 12 [l]Ee Mungu wetu, je, wewe
> hutawahukumu? Kwa kuwa sisi hatuna
> uwezo wa kukabiliana na jeshi hili
> kubwa linalokuja kutushambulia. Sisi
> hatujui la kufanya, bali macho yetu
> yanakutazama wewe.”

13 Watu wote wa Yuda pamoja na
wake zao, watoto wao na wadogo wao
wakasimama pale mbele za BWANA.

14 [m]Ndipo Roho wa BWANA akaja juu ya
mtu mmoja jina lake Yahazieli mwana wa
Zekaria, mwana wa Benaya, Mwana wa
Yeieli, mwana wa Matania, Mlawi mzao
wa Asafu alipokuwa amesimama katika
kusanyiko.

15 [n]Akasema: “Sikilizeni, enyi Yuda
wote nanyi nyote mkaao Yerusalemu,
nawe Mfalme Yehoshafati! Hili ndilo
BWANA asemalo kwenu, ‘Msiogope wala
msifadhaike kwa sababu ya jeshi hili
kubwa. Kwa maana vita hivi si vyenu, bali
ni vya Mungu. 16 Kesho shukeni kukabiliana
nao. Watakwea kwa kupandia Genge la
Sisi, nanyi mtawakuta mwisho wa bonde,
kabla ya Jangwa la Yerueli. 17 [o]Hamtahitaji
kupigana vita hivi. Kaeni kwenye nafasi
zenu, simameni imara na mkaone wokovu
BWANA atakaowapatia, enyi Yuda na

---

[a]**20:1** 1Nya 4:41
[b]**20:2** Mwa 14:7; Wim 1:14; Yos 15:62; 1Sam 23:29
[c]2 Yaani Bahari ya Chumvi.
[d]**20:3** Es 4:16; Isa 58:6; Amu 20:26; Ezr 8:21-23; 1Sam 7:6; Yer 36:9; Yn 3:5
[e]**20:4** Yoe 1:14
[f]**20:6** Mt 6:9; Kum 4:39; 1Fal 8:23; 1Nya 29:11-12; Yos 2:11; Isa 57:15; Za 47:2; 62:11; Yer 27:5; Dan 4:17; Mt 6:13
[g]**20:7** Isa 41:8; Yak 2:23; Mwa 17:7; Kut 6:7
[h]**20:8** 2Nya 6:20-28
[i]**20:9** 1Fal 8:33-37; 2Nya 6:28-29
[j]**20:10** Hes 20:14-21; Kum 2:4-6, 9, 18-19
[k]**20:11** Za 83:1-12
[l]**20:12** 2Kor 3:5; Amu 11:27; Mik 7:7; Za 12:1-2; 1Sam 3:13; Za 46:7-11; Ufu 19:11; Za 25:15
[m]**20:14** Hes 11:25; 24:2; 1Nya 12:18; 2Nya 15:1; 24:20
[n]**20:15** 2Nya 32:7; Kut 14:13-14; Za 91:8; Kum 1:29; 31:6-8
[o]**20:17** Hes 14:9; 2Nya 15:2; Kut 14:13; 2Nya 32:8; Za 46:7-11; Isa 8:10; Amo 5:14

Yerusalemu. Msiogope, wala msifadhaike.
Kesho tokeni mwende mkawakabili, naye
Bwana atakuwa pamoja nanyi.' "
18 [a]Yehoshafati akainamisha uso
wake chini, nao watu wote wa Yuda na
Yerusalemu wakaanguka chini ili kuabudu
mbele za Bwana. 19 Ndipo baadhi ya
Walawi kutoka kwa Wakohathi na kwa
wana wa Kora wakasimama na kumsifu
Bwana, Mungu wa Israeli, kwa sauti kuu
sana.
20 [b]Asubuhi na mapema wakaondoka
kuelekea Jangwa la Tekoa. Walipoanza
safari, Yehoshafati akasimama akasema,
"Nisikilizeni, enyi Yuda, na watu wa
Yerusalemu! Mwaminini Bwana Mungu
wenu, hivyo mtathibitika, wasadikini
manabii wake nanyi mtafanikiwa.
21 [c]Alipomaliza kushauriana na watu,
Yehoshafati akawaweka watu wa
kumwimbia Bwana na kumsifu katika
utukufu wa utakatifu wake walipokuwa
wametangulia mbele ya jeshi, wakisema:

"Mshukuruni Bwana
kwa kuwa upendo wake wadumu
milele."

22 [d]Walipoanza kuimba na kusifu,
Bwana akaweka waviziao dhidi ya watu
wa Amoni, Moabu na wale wa Mlima Seiri
waliokuwa wamekuja kuishambulia Yuda,
nao wakashindwa. 23 [e]Watu wa Amoni na
Moabu wakawainukia watu wa Mlima Seiri
ili kuwaua na kuwaangamiza kabisa. Baada
ya kumaliza kuwachinja watu wa Seiri,
wakaangamizana wao kwa wao.
24 [f]Yuda walipofika katika mnara wa
ulinzi wa jangwani, wakaliangalia lile jeshi
kubwa, wakaona ni maiti tupu zimetapakaa
ardhini, wala hakuna yeyote aliyenusurika.
25 Hivyo Yehoshafati na watu wake
wakaenda kujitwalia nyara kutoka kwao,
nao wakakuta humo wingi wa mifugo,
mali, nguo na vitu vya thamani, ambavyo
vilikuwa vingi zaidi ya vile walivyoweza
kuchukua. Wakakusanya nyara kwa siku
tatu kwa sababu zilikuwa nyingi mno.
26 Siku ya nne wakakusanyika katika
Bonde la Beraka[g] kwa maana huko ndiko
walikomsifu Bwana. Ndiyo sababu linaitwa
Bonde la Beraka mpaka leo.
27 [h]Kisha watu wote wa Yuda na
Yerusalemu, wakiongozwa na Yehoshafati,
wakarudi Yerusalemu wakiwa na furaha
kwa kuwa Bwana alikuwa amewasababisha
wafurahi juu ya adui zao. 28 Wakaingia
Yerusalemu na kwenda hekaluni mwa
Bwana wakiwa na vinubi, zeze na
tarumbeta.
29 [i]Hofu ya Mungu ikazipata falme
zote za nchi waliposikia jinsi Bwana
alivyokuwa amepigana dhidi ya adui za
Israeli. 30 [j]Ufalme wa Yehoshafati ukawa
na amani, kwa kuwa Mungu wake alikuwa
amemstarehesha pande zote.

### *Mwisho Wa Utawala Wa Yehoshafati*

**(1 Wafalme 22:41-50)**

31 [k]Hivyo Yehoshafati akatawala Yuda.
Alikuwa na umri wa miaka thelathini na
mitano alipoanza kutawala, akatawala
katika Yerusalemu kwa miaka ishirini na
mitano. Mama yake aliitwa Azuba binti
Shilhi. 32 Alienenda katika njia za Asa
baba yake wala hakwenda kinyume chake.
Alifanya yaliyo mema machoni pa Bwana.
33 [l]Hata hivyo mahali pa juu pa kuabudia
hapakuondolewa, na watu wakawa bado
hawajaelekeza mioyo yao kwa Mungu wa
baba zao.
34 [m]Matukio mengine ya utawala wa
Yehoshafati, kuanzia mwanzo hadi
mwisho, yameandikwa katika kitabu cha
kumbukumbu cha Yehu mwana wa Hanani,

---

[a]**20:18** Mwa 24:26; Kut 4:31
[b]**20:20** Isa 7:9; Mwa 39:3; Mit 16:3; Rum 8:31; Isa 26:3; Yn 11:40; 14:1
[c]**20:21** 1Nya 16:29; 2Nya 5:13; Za 136:1
[d]**20:22** Amu 7:22; 2Nya 13:13; 1Sam 14:20
[e]**20:23** Mwa 19:38; 2Nya 21:8; Eze 38:21
[f]**20:24** Isa 37:36; Yer 33:5; Kut 14:13

[g]26 Bonde la Beraka maana yake Bonde la Kusifu.
[h]**20:27** Neh 12:43
[i]**20:29** Mwa 35:5; Kum 2:25; 14:14; 2Nya 17:10
[j]**20:30** 2Nya 15:15; 1Nya 22:9; Ay 34:29
[k]**20:31** 1Fal 22:41
[l]**20:33** 2Nya 12:14; 17:6
[m]**20:34** 1Fal 16:1-3

ambazo zimeandikwa katika kitabu cha wafalme wa Israeli.

35 [a]Hatimaye Yehoshafati mfalme wa Yuda akafanya urafiki na Ahazia mfalme wa Israeli ambaye alifanya maovu sana. 36 [b]Akaungana naye kutengeneza meli nyingi za kwenda Tarshishi,[c] nazo zilitengenezwa huko Esion-Geberi. 37 [d]Ndipo Eliezeri mwana wa Dodavahu wa Maresha akatoa unabii dhidi ya Yehoshafati, akasema, “Kwa kuwa umeungana na Ahazia, BWANA ataangamiza vile mlivyotengeneza.” Zile meli zikavunjika na hazikuweza kung’oa nanga ili kwenda Tarshishi.

*Yehoramu Atawala*

**(2 Wafalme 8:17-24)**

21 [e]Yehoshafati akalala na baba zake, akazikwa pamoja nao katika Mji wa Daudi. Mwanawe Yehoramu akawa mfalme baada yake. 2 Ndugu zake Yehoramu, wana wa Yehoshafati walikuwa: Azaria, Yehieli, Zekaria, Azaria, Mikaeli na Shefatia. Hawa wote walikuwa wana wa Yehoshafati mfalme wa Israeli[f] 3 [g]Baba yao alikuwa amewapa zawadi nyingi za fedha na dhahabu na vitu vya thamani, pamoja na miji yenye ngome huko Yuda, bali ufalme akampa Yehoramu kwa sababu alikuwa mwanawe mzaliwa wa kwanza.

4 [h]Baada ya Yehoramu kujiimarisha katika ufalme wa baba yake, akawaua kwa upanga ndugu zake wote pamoja na baadhi ya wakuu wa Israeli. 5 Yehoramu alikuwa na umri wa miaka thelathini na miwili alipoanza kutawala, naye akatawala huko Yerusalemu kwa miaka minane. 6 [i]Akaenenda katika njia za wafalme wa Israeli, kama nyumba ya Ahabu ilivyokuwa imefanya, kwa kuwa alimwoa binti wa Ahabu. Akatenda maovu machoni pa BWANA. 7 [j]Hata hivyo, kwa sababu ya Agano ambalo BWANA alikuwa amefanya na Daudi, BWANA hakuwa radhi kuangamiza nyumba ya Daudi. Mungu alikuwa ameahidi kuidumisha taa kwa ajili yake na wazao wake milele.

8 [k]Wakati wa Yehoramu, Edomu waliasi dhidi ya Yuda na kujiwekea mfalme wao wenyewe. 9 Basi Yehoramu akaenda huko pamoja na maafisa wake na magari yake ya vita. Waedomu wakamzunguka yeye na majemadari wake wa magari yake ya vita, lakini akaondoka, akapenya usiku na kuwashambulia Waedomu. 10 [l]Hadi leo Edomu wameasi dhidi ya Yuda.

Libna pia wakaasi wakati huo huo kwa sababu Yehoramu alikuwa amemwacha BWANA, Mungu wa baba zake. 11 [m]Alikuwa pia ametengeneza mahali pa juu pa kuabudia miungu katika vilima vya Yuda na akawa amewasababisha watu wa Yerusalemu kufanya uzinzi na akawa amewapotosha watu wa Yuda.

12 [n][o]Yehoramu akapokea barua kutoka kwa nabii Eliya iliyosema:

“Hili ndilo BWANA, Mungu wa Daudi baba yako, asemalo: ‘Hukuenenda katika njia za Yehoshafati baba yako au za Asa mfalme wa Yuda. 13 [p]Lakini umeenenda katika njia za wafalme wa Israeli, nawe umewaongoza Yuda na watu wa Yerusalemu kuzini, kama vile nyumba ya Ahabu ilivyofanya. Pia umewaua ndugu zako mwenyewe, watu wa nyumbani mwa baba yako, watu waliokuwa bora kuliko wewe. 14 Hivyo basi BWANA yu karibu kuwapiga watu wako, wanao, wake zako na kila kitu

[a]**20:35** 2Nya 16:3; 19:1-3
[b]**20:36** 1Fal 22:49
[c]36 Au: za biashara (ona pia 1Fal 10:22; 22:48; 2Nya 9:21; Isa 2:16; 60:9).
[d]**20:37** 1Fal 9:26; 2Nya 9:21; Mwa 10:4; 1Fal 10:22
[e]**21:1** 1Nya 3:11
[f]2 Yaani Yuda.
[g]**21:3** 2Nya 11:23; 11:10
[h]**21:4** 1Fal 2:12; Amu 9:5; Mwa 4:8; 1Yn 3:12
[i]**21:6** 1Fal 12:28-30; 2Nya 18:1; 22:3; Neh 13:26; 2Fal 8:18
[j]**21:7** 2Sam 7:13-15; 2Nya 23:3; 2Sam 21:17; 2Fal 8:19; 1Fal 11:36; Za 132:11
[k]**21:8** 2Nya 20:22-23; Mwa 27:40; 2Fal 8:20; 9:22; Za 106:39; Ufu 17:1-5
[l]**21:10** Hes 33:20; Mwa 27:40
[m]**21:11** Law 17:7; 20:5
[n]**21:12** Kut 34:13; 1Fal 22:43
[o]**21:12** 2Fal 1:16-17; 2Nya 17:3-6; 14:2
[p]**21:13** 1Fal 16:29-33; 2:32; Kut 34:15; 2Fal 9:22

kilicho chako, kwa pigo zito. 15 [a]Wewe
mwenyewe utaugua sana kwa ugonjwa
wa tumbo kwa muda mrefu, hadi
ugonjwa utakaposababisha matumbo
yako kutoka nje.' "

16 [b]BWANA akaamsha chuki ya Wafilisti
na ya Waarabu walioishi karibu na Wakushi
dhidi ya Yehoramu. 17 [c]Wakaishambulia
Yuda, wakaivamia na kuchukua mali
zote zilizopatikana katika jumba la
mfalme pamoja na wanawe na wake zake.
Hakubakiziwa mwana yeyote isipokuwa
Ahazia aliyekuwa mdogo wa wote.
18 Baada ya mambo haya yote, BWANA
akampiga Yehoramu kwa ugonjwa
usioponyeka wa matumbo. 19 [d]Ikawa baada
ya muda, mwisho wa mwaka wa pili,
matumbo yake yakatoka nje kwa sababu
ya ugonjwa, naye akafa katika maumivu
makali sana. Watu wake hawakuwasha
moto kwa heshima yake, kama walivyokuwa
wamewafanyia baba zake.
20 [e]Yehoramu alikuwa na umri wa miaka
thelathini na miwili alipokuwa mfalme,
naye akatawala huko Yerusalemu miaka
minane. Akafa, bila kusikitikiwa na mtu
yeyote, naye akazikwa katika Mji wa Daudi,
lakini si katika makaburi ya wafalme.

*Ahazia Mfalme Wa Yuda*

**(2 Wafalme 8:25-29; 9:21-28)**

22 [f]Watu wa Yerusalemu wakamfanya
Ahazia, mdogo wa wote wa wana
wa Yerohamu, kuwa mfalme mahali pa
baba yake, kwa sababu washambuliaji wa
ghafula waliokuwa wameingia kambini
pamoja na Waarabu, walikuwa wamewaua
wana wakubwa wote wa Yehoramu. Kwa
hiyo Ahazia mwana wa Yehoramu mfalme
wa Yuda akaanza kutawala.
2 [g]Ahazia alikuwa na umri wa miaka
ishirini na miwili alipoanza kutawala, naye
akatawala katika Yerusalemu kwa mwaka
mmoja. Mama yake aliitwa Athalia, mjukuu
wa Omri.
3 [h]Ahazia naye akaenenda katika njia
za nyumba ya Ahabu, kwa sababu mama
yake alimshawishi katika kutenda maovu.
4 [i]Akafanya yaliyo maovu machoni pa
BWANA kama walivyokuwa wamefanya
nyumba ya Ahabu, kwa kuwa baada ya
kufa kwa baba yake nyumba ya Ahabu
ndio waliokuwa washauri wake, kwa
uangamivu wake. 5 [j]Pia akafuata shauri lao
alipokwenda pamoja na Yoramu mwana
wa Ahabu mfalme wa Israeli kupigana na
Hazaeli mfalme wa Aramu huko Ramoth-
Gileadi. Waaramu wakamjeruhi Yoramu.
6 [k]Hivyo akarudi Yezreeli ili apate kuuguza
majeraha aliyojeruhiwa huko Ramothi[l]
alipopigana na Hazaeli mfalme wa Aramu.
Ndipo Ahazia mwana wa Yehoramu,
mfalme wa Yuda, akashuka kwenda
Yezreeli kumtazama Yoramu mwana wa
Ahabu, kwa sababu alikuwa amejeruhiwa.
7 [m]Mungu alikuwa ameamuru kwamba
kuanguka kwa Ahazia kungetokea
atakapokwenda kumwona Yoramu. Ahazia
alipowasili, wakatoka pamoja na Yoramu
ili kwenda kukutana na Yehu mwana wa
Nimshi, ambaye BWANA alikuwa amemtia
mafuta kuangamiza nyumba ya Ahabu.
8 [n]Yehu alipokuwa anatekeleza hukumu juu
ya nyumba ya Ahabu, akawakuta wakuu
wa Yuda na wana wa jamaa ya Ahazia
waliokuwa wanamhudumia Ahazia, naye
akawaua. 9 [o]Ndipo akaenda kumsaka Ahazia,
nao watu wake wakamkamata alipokuwa
amejificha huko Samaria. Akaletwa kwa
Yehu, naye Yehu akamuua. Wakamzika
kwani walisema, "Alikuwa mwana wa

[a]**21:15** Hes 12:10
[b]**21:16** 2Nya 22:1; 26:7; 2Sam 24:1; 1Fal 11:14, 23
[c]**21:17** 2Fal 12:18; 2Nya 24:7; Yoe 3:5
[d]**21:19** 2Nya 16:14
[e]**21:20** 2Nya 33:20; Yer 22:18, 28
[f]**22:1** 2Nya 33:25; 23:20-21; 21:16-17; 26:1; 1Fal 8:24
[g]**22:2** 1Fal 16:28; 2Fal 8:26; 2Nya 21:6
[h]**22:3** 2Nya 18:1; 21:6
[i]**22:4** 2Nya 24:17; Mit 1:10; 19:27
[j]**22:5** 2Nya 18:11, 34; 2Fal 8:28
[k]**22:6** 1Fal 19:15; 2Fal 9:15
[l]6 Yaani Rama kwa Kiebrania.
[m]**22:7** Amu 14:4; 2Nya 10:15; Amo 3:6; Mdo 2:23; 2Fal 9:16; 1Fal 12:15; Za 5:10; 9:16; 1Fal 19:16
[n]**22:8** 2Fal 10:13
[o]**22:9** Amu 9:5; 2Nya 17:4; 2Fal 9:27

Yehoshafati, ambaye alimtafuta Bwana
kwa moyo wake wote." Hivyo hapakuwa
na mtu mwenye uwezo katika nyumba ya
Ahazia aliyeweza kushika ufalme.

*Athalia Na Yoashi*

**(2 Wafalme 11:1-3)**

10 Wakati Athalia mamaye Ahazia
alipoona kuwa mwanawe amekufa,
akainuka na kuiangamiza jamaa yote ya
mfalme ya nyumba ya Yuda. 11 [a]Lakini
Yehosheba, binti wa Mfalme Yehoramu,
akamtwaa Yoashi mwana wa Ahazia kwa
siri kutoka miongoni mwa wana wa mfalme
waliokuwa karibu kuuawa. Akamweka
Yoashi pamoja na yaya wake ndani ya
chumba cha kulala. Kwa kuwa Yehosheba,
aliyekuwa binti wa Mfalme Yehoramu, na
pia alikuwa mke wa kuhani Yehoyada,
alikuwa dada yake Ahazia, akamficha
huyo mtoto ili Athalia asimuue. 12 Alibaki
amefichwa pamoja nao katika Hekalu la
Mungu kwa muda wa miaka sita wakati
Athalia alikuwa akitawala nchi.

*Uasi Dhidi Ya Athalia*

**(2 Wafalme 11:4-20)**

23 [b]Katika mwaka wa saba, Yehoyada
akaonyesha nguvu zake. Alifanya
agano na wakuu wa vikosi vya mamia:
yaani Azaria mwana wa Yerohamu, Ishmaeli
mwana wa Yehohanani, Azaria mwana
wa Obedi, Maaseya mwana wa Adaya, na
Elishafati mwana wa Zikri. 2 [c]Wakazunguka
katika Yuda yote na kukusanya Walawi na
viongozi wa jamaa za Israeli kutoka miji
yote. Walipofika Yerusalemu, 3 [d]kusanyiko
lote likafanya agano na mfalme katika
Hekalu la Mungu.

Yehoyada akawaambia, "Mwana
wa mfalme atatawala, kama Bwana
alivyoahidi kuhusu wazao wa Daudi. 4 [e]Basi
hivi ndivyo iwapasavyo kufanya: Theluthi
yenu makuhani na Walawi ambao mnaingia
zamu siku ya Sabato mtalinda milangoni,
5 [f]theluthi yenu mtalinda jumba la kifalme,
na theluthi nyingine mtalinda Lango la
Msingi. Walinzi wengine wote mwe ndani
ya nyua za Hekalu la Bwana. 6 [g]Hakuna
mtu yeyote ataingia katika Hekalu la
Bwana isipokuwa makuhani na Walawi
walioko kwenye zamu. Wao wanaweza
kuingia kwa sababu ni watakatifu, lakini
watu wengine wote itawapasa kulinda
kile walichoamriwa na Bwana. 7 Walawi
watajipanga kumzunguka mfalme, kila
mtu akiwa na silaha zake mkononi. Mtu
mwingine yeyote aingiaye Hekaluni lazima
auawe. Kaeni karibu na mfalme popote
aendapo."

8 [h]Walawi na watu wote wa Yuda
wakafanya kama vile kuhani Yehoyada
aliagiza. Kila mmoja akawachukua watu
wake, wale waliokuwa wakiingia zamu siku
ya Sabato na wale waliokuwa wakienda
mapumziko, kwa sababu kuhani Yehoyada
hakuruhusu kikosi chochote kiondoke.
9 Kisha akawapa wakuu wa vikosi vya
mamia mikuki na ngao kubwa na ndogo
zilizokuwa za Mfalme Daudi, zilizokuwa
ndani ya Hekalu la Mungu. 10 Akawapanga
walinzi wote kumzunguka mfalme, kila
mmoja akiwa na silaha yake mkononi
mwake, karibu na madhabahu na Hekalu,
kuanzia upande wa kusini hadi upande wa
kaskazini mwa Hekalu.

11 [i]Yehoyada na wanawe wakamtoa
Yoashi mwana wa mfalme nje na kumvika
taji. Wakampa nakala ya agano na
kumtangaza kuwa mfalme. Wakamtia
mafuta na kupaza sauti, wakisema, "Mfalme
aishi maisha marefu!"

12 Athalia aliposikia kelele za watu
wakikimbia na kumsifu mfalme,
akawaendea watu katika Hekalu la Bwana.
13 [j]Athalia akaangalia, tazama alikuwepo
mfalme akiwa amesimama karibu na nguzo

[a]**22:11** 2Fal 11:2
[b]**23:1** 2Fal 11:4
[c]**23:2** Hes 35:2-5; Za 112:5
[d]**23:3** 2Fal 11:17; 2Sam 7:12; 1Fal 2:4; Za 89:29; 1Fal 9:5; 2Nya 6:16; 7:18; 21:7
[e]**23:4** 1Nya 9:25; Lk 1:8-9
[f]**23:5** Mdo 3:2
[g]**23:6** 1Nya 23:28-29; Hes 16:5; Zek 3:7; 2Fal 11:6-7; Ezr 8:28
[h]**23:8** 2Fal 11:9; 1Nya 24:1
[i]**23:11** Kut 25:16; Kum 17:18; 2Sam 16:16; Kut 31:18; Isa 8:16-20; 1Sam 10:24
[j]**23:13** 1Fal 1:41; 7:15; 18:17-18; Rum 2:3

yake kwenye ingilio. Maafisa na wapiga
tarumbeta walikuwa kando ya mfalme, nao
watu wote wa nchi walikuwa wanashangilia
na kupiga tarumbeta na waimbaji wakiwa
na vyombo vya uimbaji, walikuwa
wakiongoza nyimbo za sifa. Ndipo Athalia
akararua mavazi yake na kupiga kelele,
akisema, “Uhaini! Uhaini!”
14 [a]Kuhani Yehoyada akawatuma
majemadari wa vikosi vya mamia,
waliokuwa viongozi wa jeshi, na kuwaambia:
“Mleteni nje kati ya safu, na mkamuue kwa
upanga yeyote anayemfuata.” Kwa kuwa
kuhani alikuwa amesema, “Msimuulie
ndani ya Hekalu la BWANA.” 15 [b]Kwa hiyo
wakamkamata alipofika kwenye ingilio la
Lango la Farasi katika viwanja vya jumba
la mfalme wakamuulia hapo.
16 [c]Kisha Yehoyada akafanya agano
kwamba yeye na watu wote na mfalme
watakuwa watu wa BWANA. 17 [d]Kisha watu
wote wakaenda kwenye hekalu la Baali na
kulibomoa. Wakavunjavunja madhabahu
pamoja na sanamu na kumuua Matani
kuhani wa Baali mbele ya hayo madhabahu.
18 [e]Kisha Yehoyada akaweka uangalizi
wa Hekalu la BWANA mikononi mwa
makuhani, waliokuwa Walawi, ambao
Mfalme Daudi alikuwa amewagawa ili
wahudumu hekaluni kwa ajili ya kutoa
sadaka za kuteketezwa za BWANA kama
ilivyoandikwa katika Sheria ya Mose,
kwa kushangilia na kuimba kama Daudi
alivyokuwa ameagiza. 19 [f]Pia akawaweka
mabawabu kwenye malango ya Hekalu
la BWANA ili kwamba kwa vyovyote asije
akaingia mtu yeyote aliye najisi.
20 [g]Akawachukua majemadari wa
mamia, watu waheshimiwa, viongozi
wa watu pamoja na watu wote wa nchi
na kumteremsha mfalme kutoka Hekalu
la BWANA. Wakaingia kwenye jumba la
mfalme kupitia Lango la Juu na kumkalisha
mfalme kwenye kiti cha enzi, 21 [h]nao watu
wote wa nchi wakafurahi. Mji ukatulia
kwa sababu Athalia alikuwa ameuawa kwa
upanga.

*Yoashi Akarabati Hekalu*

**(2 Wafalme 12:1-16)**

24 [i]Yoashi alikuwa na umri wa miaka saba
alipoanza kutawala, naye akatawala
huko Yerusalemu kwa miaka arobaini.
Mama yake aliitwa Sibia aliyekuwa
ametoka Beer-Sheba. 2 [j]Yoashi akafanya
yaliyo mema machoni pa BWANA miaka
yote ya Yehoyada kuhani. 3 Yehoyada
akamwoza wake wawili, akazaa watoto
wa kiume na wa kike.
4 Baada ya muda, Yoashi akaamua
kukarabati Hekalu la BWANA. 5 [k]Akawaita
pamoja makuhani na Walawi akawaambia,
“Nendeni katika miji ya Yuda mkakusanye
fedha wanazopaswa kulipa kila mwaka
kutoka kwa Israeli wote, ili kukarabati
Hekalu la Mungu wenu. Fanyeni hivyo
sasa.” Lakini Walawi hawakufanya upesi.
6 [l]Kwa hiyo mfalme akamwita Yehoyada
kuhani mkuu na kumwambia, “Kwa nini
hukuwaambia Walawi walete kutoka Yuda
na Yerusalemu kodi iliyowekwa na Mose
mtumishi wa BWANA pamoja na kusanyiko
la Israeli kwa ajili ya Hema ya Ushuhuda?”
7 [m]Kwa kuwa wana wa yule mwanamke
mwovu Athalia, walikuwa wamevunja
na kuingia katika Hekalu la Mungu, nao
wakawa wamevitumia hata vile vitu
vilivyowekwa wakfu kwa BWANA kwa
mabaali.

---

[a]**23:14** Hes 5:2; 19:14
[b]**23:15** Neh 3:28; Yer 31:40; Mwa 9:5; 2Nya 22:10; Mt 7:2
[c]**23:16** 2Nya 34:31; Neh 9:38; 2Nya 15:12; Kum 5:2-3; 2Fal 11:17; 2Nya 19:10; Ezr 10:3
[d]**23:17** Kum 13:6-9; 2Fal 10:23; 11:18; 18:4; 2Nya 34:4-7
[e]**23:18** 1Nya 23:28-32; 2Nya 5:5; Kut 29:38; Hes 28:2; 1Nya 23:6
[f]**23:19** 1Nya 9:22
[g]**23:20** 2Fal 15:25; 11:19
[h]**23:21** 2Nya 22:1; 1Sam 11:15; Za 58:10; Mit 11:10; 1Fal 1:40; 2Fal 11:20; Mit 29:2
[i]**24:1** 2Fal 11:21; 12:1
[j]**24:2** 2Nya 25:2; 26:5
[k]**24:5** Kut 30:16; Mt 17:24; 1Nya 26:20; 11:1; 2Fal 12:4; 2Nya 29:3; 34:8
[l]**24:6** Kut 35:21; Hes 1:50; Mdo 7:44; Hes 17:7-8; Kut 30:12-16; 2Fal 12:7
[m]**24:7** 2Nya 21:17; 22:3-4; Za 12:8

8 [a]Kwa amri ya mfalme, likatengenezwa
kasha, nalo likawekwa nje kwenye lango
la Hekalu la BWANA. 9 [b]Tangazo likatolewa
katika Yuda na Yerusalemu kwamba inapasa
wamletee BWANA kodi ile ambayo Mose,
mtumishi wa BWANA alikuwa amewaagiza
Israeli huko jangwani. 10 [c]Maafisa wote
na watu wote wakaleta michango yao
kwa furaha, wakaweka kwenye kasha
mpaka likajaa. 11 [d]Ikawa kila wakati kasha
lilipoletwa ndani na Walawi kwa maafisa
wa mfalme na kuona kwamba kuna
kiasi kikubwa cha fedha, mwandishi wa
mfalme na afisa wa kuhani mkuu walikuwa
wanakuja na kumimina, kisha kulirudisha
mahali pake. Walifanya hivi mara kwa
mara, nao wakakusanya fedha nyingi sana.
12 [e]Mfalme na Yehoyada wakawapa wale
watu waliofanya kazi iliyotakiwa katika
Hekalu la BWANA. Wakawaajiri waashi
na maseremala ili kutengeneza Hekalu
la BWANA, pia wafanyakazi za chuma na
shaba ili kukarabati Hekalu la BWANA.
13 [f]Watu walioshughulika na kazi
walikuwa wenye bidii, nayo kazi ya
kukarabati ikaendelea vizuri mikononi
mwao. Wakalitengeneza upya Hekalu la
BWANA likarudi katika hali yake ya awali
na kuliimarisha. 14 [g]Walipokamilisha
kazi hiyo ya kukarabati, wakaleta fedha
zilizobaki wakampa mfalme na Yehoyada,
nao kwa hizo wakatengeneza vyombo kwa
ajili ya Hekalu la BWANA: Vyombo kwa
ajili ya huduma na kwa ajili ya sadaka
ya kuteketezwa, pia mabakuli na vitu
vingine vya dhahabu na fedha. Wakati
wote Yehoyada alipokuwa hai, sadaka za
kuteketezwa zilitolewa wakati wote katika
Hekalu la BWANA.
15 [h]Basi Yehoyada alikuwa mzee
aliyeshiba siku wakati alipofariki. Alikufa
akiwa na umri wa miaka 130. 16 [i]Wakamzika
pamoja na wafalme katika Mji wa Daudi,
kwa sababu ya mema aliyokuwa ametenda
katika Israeli kwa ajili ya Mungu na Hekalu
lake.

*Uovu Wa Yoashi*

17 [j]Baada ya kifo cha Yehoyada, wakuu
wa Yuda walikuja kumpa mfalme heshima,
naye akawasikiliza. 18 [k]Wakaacha Hekalu la
BWANA, Mungu wa baba zao, wakaabudu
nguzo za maashera na sanamu. Kwa
sababu ya hatia yao, hasira ya Mungu
ikawajia Yuda na Yerusalemu. 19 [l]Ingawa
BWANA aliwatuma manabii wawarudishe
watu kwake na ingawa waliwaonya,
hawakuwasikiliza.
20 [m]Ndipo Roho wa BWANA akaja juu
ya Zekaria mwana wa Yehoyada kuhani.
Akasimama mbele ya watu akasema, "Hili
ndilo asemalo Mungu, 'Kwa nini mnakataa
kuzitii amri za BWANA? Hamtafanikiwa
kwa kuwa mmemwacha BWANA, yeye naye
amewaacha ninyi.' "
21 [n]Lakini wakafanya shauri baya juu
yake na kwa amri ya mfalme wakampiga
kwa mawe mpaka akafa katika ukumbi
wa Hekalu la BWANA. 22 [o]Mfalme Yoashi
hakukumbuka wema aliotendewa na
Yehoyada baba yake Zekaria ila alimuua
mwanawe, ambaye alisema wakati akiwa
amelala akingojea kufa, "BWANA na alione
hili na alipize kisasi."
23 [p]Mwishoni mwa ule mwaka, jeshi la
Waaramu likaja dhidi ya Yoashi, likavamia
Yuda na Yerusalemu na kuwaua viongozi

[a]**24:8** 2Fal 12:9
[b]**24:9** Kut 36:6
[c]**24:10** Kut 25:2; 1Nya 29:3-9
[d]**24:11** 2Fal 12:10
[e]**24:12** 2Nya 34:11
[f]**24:13** Neh 4:7
[g]**24:14** 1Fal 7:50; 2Fal 12:13; Kut 29:38; Ebr 7:27; 1Pet 1:18-19; Ufu 5:9
[h]**24:15** Ay 5:26
[i]**24:16** 1Fal 2:10
[j]**24:17** Mdo 20:29
[k]**24:18** Yos 24:20; 1Fal 14:23; Yer 17:2; Yos 22:20; 2Nya 19:2; Amu 5:8; 2Sam 24:1; 2Nya 28:13; Hos 5:10
[l]**24:19** Hes 11:29; Zek 1:4; 2Nya 36:15; Neh 9:26; Yer 7:25-26; 25:4; Lk 11:47-51
[m]**24:20** Amu 3:10; Mt 23:35; 1Nya 12:18; Hes 14:41; 2Nya 15:2; Kum 31:17; 2Nya 15:1-2; Amu 6:34; 1Sam 13:13-14; Kum 29:25-26; Yer 2:19
[n]**24:21** Yos 7:25; Mdo 7:58-59; Neh 9:26; Yer 26:21; 20:2; Mt 23:35
[o]**24:22** Mwa 9:5
[p]**24:23** 2Fal 12:17-18

wote wa watu. Wakapeleka nyara zao zote
kwa mfalme wao huko Dameski. 24 [a]Ingawa
jeshi la Waaramu lilikuwa limekuja na watu
wachache tu, BWANA akatia mikononi
mwao jeshi kubwa kuliko lao. Kwa sababu
Yuda walikuwa wamemwacha BWANA,
Mungu wa baba zao, hukumu ilitekelezwa
juu ya Yoashi. 25 [b]Waaramu walipoondoka,
walimwacha Yoashi akiwa mgonjwa sana.
Maafisa wake wakafanya hila dhidi yake
kwa sababu alikuwa amemuua mwana
wa Kuhani Yehoyada, nao wakamuulia
kitandani mwake. Hivyo akafa na
wakamzika katika Mji wa Daudi, lakini si
katika makaburi ya wafalme.

26 [c]Wale waliofanya hila mbaya dhidi yake
walikuwa Zabadi, mwana wa Shimeathi
mwanamke Mwamoni, Yehozabadi, mwana
wa Shimrithi mwanamke Mmoabu. 27 Kwa
habari za wanawe, unabii mwingi kumhusu
na kumbukumbu za kutengenezwa upya
kwa Hekalu la Mungu, zimeandikwa katika
kitabu cha kumbukumbu za wafalme.
Amazia mwanawe akawa mfalme baada
yake.

### *Amazia Mfalme Wa Yuda*

**(2 Wafalme 14:2-20)**

25 [d]Amazia alikuwa na umri wa miaka
ishirini na mitano alipoanza kutawala,
naye akatawala huko Yerusalemu kwa
miaka ishirini na tisa. Mama yake aliitwa
Yehoadani kutoka Yerusalemu. 2 [e]Akatenda
yaliyo mema machoni pa BWANA, lakini sio
kwa moyo wake wote. 3 [f]Baada ya ufalme
kuimarika mikononi mwake, aliwaua
maafisa waliomuua mfalme baba yake.
4 [g]Hata hivyo hakuwaua watoto wao, lakini
akafanya sawasawa na ilivyoandikwa katika
Sheria, katika Kitabu cha Mose, ambako
BWANA aliamuru: "Baba hawatauawa
kwa ajili ya watoto wao, wala watoto
hawatauawa kwa ajili ya baba zao. Kila
mmoja atakufa kwa ajili ya dhambi zake
mwenyewe."

5 [h]Amazia akawaita watu wa Yuda
pamoja, akawaweka chini ya majemadari
wa maelfu na majemadari wa mamia
kufuatana na jamaa zao katika Yuda yote na
Benyamini. Kisha akawahesabu wale wenye
umri wa miaka ishirini au zaidi na akakuta
kwamba walikuwa wanaume 300,000 watu
walio tayari kwa utumishi wa jeshi, walio
na uwezo wa kutumia mkuki na ngao.
6 Akawaajiri pia watu 100,000 wapiganaji
kutoka Israeli kwa talanta 100 za fedha.[i]

7 [j]Lakini mtu wa Mungu akamjia na
kumwambia, "Ee mfalme, haya majeshi
kutoka Israeli kamwe usiyaruhusu yaende
pamoja na wewe kwa kuwa BWANA hayuko
pamoja na Israeli, wala hayupo pamoja na
yeyote wa watu wa Efraimu. 8 [k]Hata kama
ukienda na kupigana kwa ujasiri katika vita,
Mungu atakufanya ukimbie mbele ya adui,
kwa kuwa Mungu anao uwezo wa kusaidia
au wa kuangusha."

9 [l]Amazia akamuuliza yule mtu wa
Mungu, "Lakini itakuwaje kwa zile talanta
100 za fedha nilizolipa kwa ajili ya haya
majeshi ya Israeli?"

Yule mtu wa Mungu akajibu, "BWANA
aweza kukupa zaidi sana ya hizo."

10 Hivyo Amazia akayaondoa yale majeshi
yaliyokuwa yamekuja kutoka Efraimu na
kuyarudisha nyumbani. Waliwakasirikia
sana Yuda, nao wakarudi nyumbani wakiwa
na hasira kali.

11 [m]Ndipo Amazia akajitia nguvu na
kuliongoza jeshi lake kwenye Bonde la
Chumvi, ambako aliua watu 10,000 wa

---

[a]**24:24** 2Nya 14:9; Law 26:23-25; Kum 28:25; 32:30; Isa 10:5; 30:17
[b]**24:25** 2Nya 21:20; 2Fal 12:18-20; Za 10:14
[c]**24:26** 2Fal 12:21; Rut 1:4
[d]**25:1** 2Fal 14:1
[e]**25:2** 1Fal 8:61; Isa 29:13; 2Fal 14:4; Isa 29:13; Hos 10:2
[f]**25:3** 2Fal 14:5
[g]**25:4** Kum 28:61; Hes 26:11; Kum 24:16; Eze 18:20; 2Fal 14:6; Yer 31:30
[h]**25:5** 2Sam 24:2; Kut 30:14; 1Nya 21:1
[i]6 Talanta 100 za fedha ni sawa na tani 3.75.
[j]**25:7** 2Nya 16:2-9; 19:1-3; Hos 4:6-19; 1Fal 12:28; Isa 28:1-3; Hos 5:6-15; 9:11-17
[k]**25:8** 2Nya 14:11; 20:6; Mwa 18:14; Amu 7:7; 1Sam 14:6; 1Nya 29:11; Ay 5:18; Za 20:7; 118:6; Yer 32:17; Mt 19:26; Rum 8:31
[l]**25:9** Kum 8:18; Mit 10:22; Hag 2:8; 2Nya 1:12
[m]**25:11** 2Fal 14:7

Seiri. 12 [a]Jeshi la Yuda pia likawateka watu
10,000 wakiwa hai, likawapandisha juu ya
jabali na kuwatupa chini kwa nguvu hata
wote wakavunjika vipande vipande.
13 Wakati huo yale majeshi Amazia
aliyoyarudisha na ambayo hakuyaruhusu
kushiriki katika vita, yalivamia miji ya
Yuda kuanzia Samaria hata Beth-Horoni.
Yakawaua watu 3,000 na kuchukua kiasi
kikubwa sana cha mateka.
14 [b]Amazia aliporudi kutoka kuwachinja
Waedomu, alileta pia kutoka huko miungu
ya watu wa Seiri. Akaisimamisha kama
miungu yake mwenyewe, akaisujudia na
kuitolea kafara za kuteketezwa. 15 [c]Hasira
ya BWANA ikawaka dhidi ya Amazia, naye
akamtuma nabii kwake, ambaye alisema:
“Kwa nini unauliza kwa miungu ya hawa
watu, ambayo haikuweza kuwaokoa watu
wake wenyewe kutoka mkononi mwako?”
16 [d]Wakati nabii alipokuwa angali
anazungumza, mfalme akamwambia, “Je,
wewe tumekuchagua kuwa mshauri wa
mfalme? Nyamaza, ya nini uuawe?”
Hivyo nabii akanyamaza lakini
akasema, “Najua kuwa Mungu ameazimia
kukuangamiza kwa sababu umefanya jambo
hili na hukusikiliza shauri langu.”
17 [e]Baada ya Amazia mfalme wa Yuda
kushauriana na washauri wake akatuma
ujumbe kwa Yehoashi, mwana wa
Yehoahazi mwana wa Yehu, mfalme wa
Israeli kusema: “Njoo tukabiliane uso kwa
uso.”
18 [f]Lakini Yehoashi mfalme wa Israeli
akamjibu Amazia mfalme wa Yuda,
“Mbaruti uliokuwa Lebanoni ulituma
ujumbe kwa mwerezi uliokuwa Lebanoni,
‘Mtoe binti yako aolewe na mwanangu.’
Kisha mnyama wa mwituni aliyekuwa
Lebanoni akaja na kuukanyaga ule mbaruti.
19 [g]Wewe unasema moyoni mwako kwamba
umemshinda Edomu, nawe sasa unajigamba
na kujivuna. Lakini kaa nyumbani kwako!
Kwa nini utafute matatizo na kujiletea
anguko lako mwenyewe na la Yuda pia?”
20 [h]Hata hivyo, Amazia hakutaka
kusikia, kwa kuwa Mungu alifanya hivyo
ili awatie mikononi mwa Yehoashi, kwa
sababu waliitafuta miungu ya Edomu.
21 Hivyo Yehoashi mfalme wa Israeli
akakwea kuwashambulia. Yeye na Amazia
mfalme wa Yuda wakakabiliana uso kwa
uso huko Beth-Shemeshi katika Yuda.
22 Yuda ikashindwa na Israeli na kila mtu
akakimbilia nyumbani kwake. 23 [i]Yehoashi
mfalme wa Israeli akamteka Amazia
mfalme wa Yuda, mwana wa Yoashi,
mwana wa Ahazia, huko Beth-Shemeshi.
Kisha Yehoashi akamleta Yerusalemu na
kuubomoa ukuta wa Yerusalemu kuanzia
lango la Efraimu hadi Lango la Pembeni,
sehemu yenye urefu wa kama dhiraa
400.[j] 24 [k]Akachukua dhahabu yote, fedha
na vyombo vyote vilivyopatikana katika
Hekalu la Mungu, ambavyo vilikuwa chini
ya uangalizi wa Obed-Edomu, pamoja na
hazina za jumba la mfalme na mateka, kisha
akarudi Samaria.
25 [l]Amazia mwana wa Yoashi mfalme
wa Yuda aliishi miaka kumi na mitano
baada ya kifo cha Yehoashi mwana wa
Yehoahazi mfalme wa Israeli. 26 Kwa habari
ya matukio mengine katika utawala wa
Amazia, kuanzia mwanzo hadi mwisho, je,
hayakuandikwa katika kitabu cha wafalme
wa Yuda na wa Israeli? 27 [m]Kuanzia wakati
ule Amazia alipogeuka na kuacha kumfuata
BWANA walifanya shauri baya dhidi yake
huko Yerusalemu naye akakimbilia Lakishi,
lakini wakawatuma watu wamfuatilie
huko Lakishi nao wakamuulia huko.
28 [n]Akarudishwa kwa farasi na akazikwa
pamoja na baba zake katika Mji wa Yuda.

[a]**25:12** Za 141:6; Oba 1:3
[b]**25:14** Kut 20:3; Isa 36:20; 2Nya 28:23
[c]**25:15** Yer 10:3-5; Mdo 19:26; Za 96:5; 115:3-8; Isa 46:1-2; 1Kor 8:4
[d]**25:16** 2Nya 16:10; Mit 9:7-8; 1Sam 2:25
[e]**25:17** 2Fal 14:8-9
[f]**25:18** Amu 9:8-15
[g]**25:19** 2Nya 35:21; Mit 18:9; 12:15
[h]**25:20** 1Fal 12:15; 2Nya 22:7
[i]**25:23** 2Fal 14:13; Neh 8:16; 2Nya 26:9; Yer 31:38; 2Nya 21:17; 22:1, 6
[j]23 Dhiraa 400 ni sawa na mita 180.
[k]**25:24** 1Nya 26:15
[l]**25:25** 2Fal 14:17
[m]**25:27** Yos 10:3
[n]**25:28** 2Fal 14:20

*Uzia Mfalme Wa Yuda*

**(2 Wafalme 14:21-22; 15:1-7)**

26 [a]Kisha watu wote wa Yuda wakamtwaa
Uzia, aliyekuwa na umri wa miaka
kumi na sita, nao wakamfanya mfalme
mahali pa Amazia baba yake. 2 Ndiye
alijenga upya Elathi kuirudisha kwa Yuda
baada ya Amazia kulala pamoja na baba
zake.

3 Uzia alikuwa na umri wa miaka kumi
na sita alipoanza kutawala, naye akatawala
huko Yerusalemu kwa miaka hamsini na
miwili. Mama yake aliitwa Yekolia wa
Yerusalemu. 4 Akatenda yaliyo mema
machoni pa Bwana, kama Amazia baba
yake alivyofanya. 5 [b]Akamtafuta Mungu
katika siku za Zekaria, aliyemwelekeza
kumcha Mungu. Wakati wote alipomtafuta
BWANA, Mungu alimfanikisha.

6 [c]Alipigana vita dhidi ya Wafilisti na
kubomoa kuta za Gathi, Yabne na Ashdodi.
Kisha akajenga upya miji karibu na Ashdodi
na mahali pengine katikati ya Wafilisti.
7 [d]Mungu akamsaidia dhidi ya Wafilisti na
dhidi ya Waarabu walioishi Gur-Baali na
dhidi ya Wameuni. 8 [e]Waamoni wakamletea
Uzia ushuru, umaarufu wake ukaenea
hadi kwenye mpaka wa Misri, kwa sababu
alikuwa amekuwa na nguvu sana.

9 [f]Uzia akajenga minara huko Yerusalemu
katika Lango la Pembeni, katika Lango la
Bondeni na katika pembe, mahali kuta
zikutanapo, kisha akaijengea ngome.
10 [g]Akajenga pia minara jangwani na
kuchimba visima vingi vya maji, kwa
sababu alikuwa na mifugo mingi chini
ya vilimani na kwenye nchi tambarare.
Alikuwa na watu wanaofanya kazi katika
mashamba yake na kwenye mashamba yake
ya mizabibu huko vilimani na katika ardhi
zenye rutuba, kwa kuwa aliupenda udongo.

11 Zaidi ya hayo, Uzia alikuwa na jeshi
lililofunzwa vizuri, lililokuwa tayari
kwenda vitani kwa vikosi kufuatana na
idadi yao kama walivyokusanywa na Yeieli
mwandishi na Maaseya msimamizi chini
ya maelekezo ya Hanania, mmojawapo
wa maafisa wa mfalme. 12 Idadi yote ya
viongozi wa jamaa waliowaongoza hawa
wapiganaji walikuwa 2,600. 13 Chini ya
uongozi wao kulikuwa na jeshi la askari
307,500 watu waliofundishwa kwa ajili ya
vita, jeshi lenye nguvu la kumsaidia mfalme
dhidi ya adui zake. 14 [h]Uzia akalipatia jeshi
lote ngao, mikuki, chapeo, dirii, pinde na
mawe ya kombeo. 15 Huko Yerusalemu watu
wenye utaalamu mkubwa wakatengeneza
mitambo iliyotumika katika minara na
kwenye pembe za ulinzi ili kurusha mishale
na kuvurumisha mawe makubwa. Sifa zake
zikaenea mbali sana kwa sababu alisaidiwa
mno mpaka akawa na nguvu sana.

16 [i]Lakini baada ya Uzia kuwa na nguvu
sana, majivuno yake yakamsababishia
kuanguka. Alikosa uaminifu kwa BWANA
Mungu wake, naye akaingia hekaluni
mwa BWANA ili afukize uvumba kwenye
madhabahu ya kufukizia uvumba. 17 [j]Azaria
kuhani akiwa pamoja na makuhani wengine
themanini wa BWANA wenye ujasiri
wakamfuata huko ndani. 18 [k]Wakamkabili
na kumwambia, "Siyo sawa kwako, Uzia,
kumfukizia BWANA uvumba. Hiyo ni kazi
ya makuhani, wazao wa Aroni, ambao
wamewekwa wakfu ili kufukiza uvumba.
Ondoka mahali patakatifu, kwa kuwa
umekosa uaminifu nawe hutaheshimiwa
na BWANA."

19 [l]Uzia, ambaye alikuwa na chetezo
mkononi mwake tayari kufukiza uvumba,

---

[a]**26:1** 1Fal 14:21; 2Nya 22:1
[b]**26:5** 2Nya 15:2; Mwa 41:15; Dan 1:17; 2Nya 7:2; Dan 2:9; 10:1
[c]**26:6** Isa 2:6; Yer 25:20; Amo 3:9; Isa 14:29; 1Nya 21:16
[d]**26:7** 2Nya 21:16; 1Nya 5:20; 2Nya 20:1; 14:11; Mdo 26:22
[e]**26:8** Mwa 19:38; 2Nya 17:11; 1Sam 11:1; 2Sam 8:2
[f]**26:9** 2Fal 14:13; 2Nya 25:23; Neh 2:13; 3:13; Zek 14:10
[g]**26:10** 2Nya 21:16
[h]**26:14** Yer 46:4
[i]**26:16** 2Fal 14:10; Kum 32:15; 2Nya 25:19; 1Nya 5:25; 2Fal 16:12-13; Hab 2:4; Kol 2:18; Kum 8:14
[j]**26:17** 1Nya 6:10; 1Fal 4:2; Mdo 26:22
[k]**26:18** Hes 16:39; 18:1-7; Kut 30:7; Yer 13:18; 1Nya 6:49; 2Nya 19:2; Mt 14:4; Gal 2:21
[l]**26:19** 2Fal 5:25-27; Hes 12:10

akakasirika. Alipokuwa anawaghadhibikia
makuhani mbele ya madhabahu ya
kufukizia uvumba katika Hekalu la BWANA,
ukoma ukamtokea penye kipaji chake cha
uso. 20 [a]Azaria kuhani mkuu pamoja na
makuhani wengine wote walipomtazama
wakaona kwamba alikuwa na ukoma penye
kipaji chake cha uso wakaharakisha kumtoa
nje. Naam, hata yeye mwenyewe alikuwa
anatamani kuondoka kwa sababu BWANA
alikuwa amempiga.

21 [b]Mfalme Uzia alikuwa na ukoma
mpaka siku ya kufa kwake. Akatengwa
katika nyumba ya pekee akiwa mwenye
ukoma, naye akawa ametengwa kutoka
Hekalu la BWANA. Yothamu mwanawe
akawa msimamizi wa jumba la mfalme,
pia akawaongoza watu wa nchi.

22 [c]Matukio mengine ya utawala wa
Uzia, kuanzia mwanzo mpaka mwisho,
yameandikwa na nabii Isaya mwana wa
Amozi. 23 [d]Uzia akalala pamoja na baba zake,
naye akazikwa karibu nao katika shamba
la kuzikia lililokuwa mali ya wafalme, kwa
kuwa watu walisema, "Alikuwa na ukoma."
Yothamu mwanawe akawa mfalme baada
yake.

### *Yothamu Mfalme Wa Yuda*

**(2 Wafalme 15:32-38)**

27 [e]Yothamu alikuwa na umri wa miaka
ishirini na mitano alipoanza kutawala,
naye akatawala huko Yerusalemu miaka
kumi na sita. Mama yake aliitwa Yerusha
binti Sadoki. 2 [f]Akafanya yaliyo mema
machoni pa BWANA kama Uzia baba yake
alivyokuwa amefanya, lakini tofauti na
yeye, hakuingilia huduma za hekaluni
mwa BWANA. Lakini hata hivyo, watu
wakaendelea na desturi zao mbaya.
3 [g]Yothamu akajenga upya Lango la Juu la
Hekalu la BWANA na kufanya kazi kubwa
kwenye ukuta katika kilima cha Ofeli.
4 Akajenga miji katika vilima vya Yuda
pamoja na ngome na minara mwituni.

5 [h]Yothamu akafanya vita na mfalme
wa Waamoni na kumshinda. Mwaka ule
Waamoni wakamlipa talanta 100[i] za fedha,
kori 10,000[j] za ngano na kori 10,000 za
shayiri. Waamoni wakamletea kiasi hicho
hicho mwaka wa pili na wa tatu.

6 [k]Yothamu akaendelea kuwa na nguvu
kwa sababu alienenda kwa ukamilifu mbele
za BWANA Mungu wake.

7 Matukio mengine ya utawala wa
Yothamu, pamoja na vita vyake vyote na
vitu vingine alivyofanya, vimeandikwa
katika kitabu cha wafalme wa Israeli na
Yuda. 8 Alikuwa na umri wa miaka ishirini
na mitano alipoanza kutawala, naye
akatawala huko Yerusalemu miaka kumi
na sita. 9 Yothamu akalala na baba zake na
akazikwa katika Mji wa Daudi. Naye Ahazi
mwanawe akawa mfalme baada yake.

### *Ahazi Mfalme Wa Yuda*

**(2 Wafalme 16:1-6)**

28 [l]Ahazi alikuwa na miaka ishirini
alipoanza kutawala. Akatawala huko
Yerusalemu kwa miaka kumi na sita. Tofauti
na Daudi baba yake, hakufanya yaliyo
mema machoni pa BWANA. 2 [m]Akaenenda
katika njia za wafalme wa Israeli, na pia
akasubu sanamu kwa ajili ya kuabudu
Mabaali. 3 [n]Akatoa sadaka za kuteketezwa
katika Bonde la Ben-Hinomu, na kuwatoa
wanawe kafara kwa kuwateketeza kwa
moto, akifuata njia za machukizo za yale
mataifa BWANA aliyoyafukuza humo mbele
ya Waisraeli. 4 Akatoa sadaka na kufukiza
uvumba katika mahali pa juu pa kuabudia

---

[a] **26:20** Es 6:12
[b] **26:21** Law 13:46; 14:8; Kut 4:6; 2Fal 15:5; Hes 5:2
[c] **26:22** 2Fal 15:1; Isa 6:1
[d] **26:23** 2Fal 15:7; Isa 6:1
[e] **27:1** 1Fal 15:5, 32; 1Nya 3:12; Isa 1:1; Hos 1:1; Mik 1:1
[f] **27:2** 2Nya 26:16-21; Za 119:120; 2Fal 15:35
[g] **27:3** 2Nya 26:16-21; 33:14; Neh 3:26
[h] **27:5** 2Nya 26:8; Mwa 19:36; Yer 49:1-6; 2Fal 3:4
[i] 5 Talanta 100 za fedha ni sawa na tani 3.75.
[j] 5 Kori 10,000 za ngano ni sawa na tani 2.2.
[k] **27:6** 2Nya 26:5; 1Sam 2:30; 1Nya 12:14; 19:3; Za 34:8; 40:4
[l] **28:1** 2Fal 16:2; 1Nya 3:13
[m] **28:2** Kut 34:17; 2Nya 22:3; Law 19:4
[n] **28:3** Yos 15:8; 2Fal 23:10; Law 18:21; Eze 20:26; Kum 18:9; 2Nya 33:2

miungu, juu ya vilima, na chini ya kila mti
uliotanda.
5 [a]Kwa hiyo BWANA Mungu wake
akamtia mikononi mwa mfalme wa Aramu.
Waaramu wakamshinda, wakachukua watu
wake wengi mateka na kuwaleta mpaka
Dameski.
Tena alitiwa mikononi mwa mfalme wa
Israeli, ambaye aliwaua watu wake wengi.
6 [b]Kwa siku moja Peka mwana wa Remalia
aliwaua askari 120,000 katika Yuda,
kwa kuwa Yuda walikuwa wamemwacha
BWANA, Mungu wa baba zao. 7 Zikri,
askari shujaa Mwefraimu, akamuua
Maaseya mwana wa mfalme, Azrikamu
mkuu wa jumba la kifalme na Elikana
aliyekuwa wa pili kwa mfalme. 8 [c]Waisraeli
wakawachukua mateka kutoka ndugu zao,
watu wapatao 200,000 hawa wakiwa ni
wanawake, watoto wa kiume na wa kike.
Wakachukua pia kiasi kikubwa cha nyara,
ambazo walirudi nazo Samaria.
9 [d]Lakini kulikuwako huko nabii wa
BWANA aliyeitwa Odedi, akaondoka ili
kukutana na jeshi liliporejea Samaria.
Akawaambia, "Kwa kuwa BWANA,
Mungu wa baba zenu, aliwakasirikia
Yuda, aliwatia mikononi mwenu. Lakini
mmewachinja kwa hasira ambayo imefika
hadi mbinguni. 10 [e]Nanyi sasa mnakusudia
kuwafanya wanaume na wanawake wa
Yuda na Yerusalemu watumwa wenu.
Lakini ninyi je, hamna pia hatia ya dhambi
mliyotenda dhidi ya BWANA Mungu wenu?
11 [f]Basi nisikilizeni! Mkawarudishe mateka
mliowachukua kutoka kwa ndugu zenu,
kwa kuwa hasira kali ya BWANA iko juu
yenu."
12 Ndipo baadhi ya viongozi katika
Efraimu, yaani, Azaria mwana wa
Yehohanani, Berekia mwana wa
Meshilemothi, Yehizkia mwana wa
Shalumu na Amasa mwana wa Hadlai,
wakakubaliana na huyo nabii, hivyo
wakawapinga wale waliokuwa wanawasili
kutoka vitani. 13 [g]Wakamwambia, "Hamna
ruhusa kuwaleta hao wafungwa hapa, ama
sivyo tutakuwa na hatia mbele za BWANA.
Je, mnataka kuongezea dhambi yetu na
hatia yetu? Kwa sababu hatia yetu tayari
ni kubwa, nayo hasira kali ya BWANA iko
juu ya Israeli."
14 Hivyo wale askari wakawaacha wale
mateka pamoja na nyara mbele ya hao
maafisa na kusanyiko lote. 15 [h]Kisha watu
waliotajwa kwa majina wakawachukua wale
mateka na kutoka zile nyara, wakachukua
mavazi wakawavika wale wafungwa wote
waliokuwa uchi. Wakawapatia nguo na
viatu, chakula na cha kunywa, wakawapa
matibabu, wote waliokuwa dhaifu miongoni
mwao wakawapandisha juu ya punda,
wakawaleta ndugu zao mpaka Yeriko, ndio
Mji wa Mitende, kisha wakarudi Samaria.

### *Waashuru Wakataa Kusaidia Yuda*

### (2 Wafalme 16:7-9)

16 [i]Wakati ule, Mfalme Ahazi akatuma
wajumbe kwa mfalme wa Ashuru
kuomba msaada. 17 [j]Waedomu walikuwa
wamekuja tena na kuwashambulia Yuda na
kuchukua mateka. 18 Pia Wafilisti walikuwa
wameshambulia miji iliyokuwa chini ya
vilima na katika miji ya Negebu ya Yuda.
Nao wakawa wametwaa Beth-Shemeshi,
Aiyaloni, Gederothi, Soko pamoja na vijiji
vyake, Timna pamoja na vijiji vyake, Gimzo
pia pamoja na vijiji vyake na kuishi humo.
19 [k]BWANA aliishusha Yuda kwa sababu ya
Ahazi mfalme wa Israeli, kwa kuwa alikuwa
ameongeza uovu katika Yuda na kumkosea
BWANA mno. 20 [l]Hivyo Tiglath-Pileseri
mfalme wa Ashuru akaja kumtesa badala
ya kumsaidia. 21 Ahazi akachukua baadhi

[a]**28:5** Isa 7:1
[b]**28:6** 2Fal 15:25-27; Isa 11:13; Yer 2:19
[c]**28:8** Kum 28:25-41; 2Nya 11:4; 29:9
[d]**28:9** Isa 10:6; Zek 1:15; Ezr 9:6; Ufu 18:5; Amu 3:5
[e]**28:10** Law 25:39-46; Yer 25:29
[f]**28:11** 2Nya 11:4; Yak 2:13
[g]**28:13** Hes 32:14; Yos 22:17
[h]**28:15** 2Fal 6:22; Mit 25:21-22; Kum 34:3; Amu 1:16; Lk 6:27; Rum 12:20
[i]**28:16** 2Fal 16:7; Eze 23:12; Isa 7:1-9
[j]**28:17** Law 26:18; Isa 63:1; Eze 25:12; 2Nya 29:9
[k]**28:19** 1Nya 5:25; 2Nya 21:2; Ufu 16:15
[l]**28:20** 2Fal 15:29; 1Nya 5:6; 2Fal 16:7-9; Isa 7:20

ya vitu kutoka Hekalu la BWANA, jumba la kifalme na kutoka kwa wakuu wake na kumpa mfalme wa Ashuru kama ushuru, lakini hilo halikumsaidia.

[22] [a]Katika wakati wake wa mateso Mfalme Ahazi akazidi kukosa uaminifu kwa BWANA. [23] [b]Akatoa kafara kwa miungu ya Dameski, waliokuwa wamemshinda, kwa kuwa aliwaza, “Kwa kuwa miungu ya mfalme wa Aramu imewasaidia wao, nitaitolea dhabihu ili inisaidie na mimi.” Lakini haya ndiyo yaliyokuwa maangamizi yake na Israeli wote.

[24] [c]Ahazi akakusanya pamoja vyombo vya nyumba ya Mungu na kuvivunja vipande vipande. Akafunga milango ya Hekalu la BWANA na kusimamisha madhabahu katika kila njia panda ya barabara za Yerusalemu. [25] Katika kila mji wa Yuda akajenga mahali pa juu pa kuabudia miungu ili kutolea miungu mingine kafara za kuteketezwa na kuchochea hasira ya BWANA, Mungu wa baba zake.

[26] [d]Matukio mengine ya utawala wake na njia zake nyingine zote, tangu mwanzo hadi mwisho, zimeandikwa katika kitabu cha wafalme wa Yuda na Israeli. [27] [e]Ahazi akalala na baba zake na akazikwa katika Mji wa Yerusalemu, lakini hawakumleta kwenye makaburi ya wafalme wa Israeli. Naye Hezekia mwanawe akawa mfalme baada yake.

*Hezekia Mfalme Wa Yuda*

**(2 Wafalme 18:1-12)**

29 [f]Hezekia alikuwa na umri wa miaka ishirini na mitano alipoanza kutawala, naye akatawala huko Yerusalemu kwa miaka ishirini na tisa. Mama yake aliitwa Abiya binti Zekaria. [2] [g]Akafanya yaliyo mema machoni pa BWANA kama Daudi baba yake alivyofanya.

[3] [h]Katika mwezi wa kwanza wa mwaka wa kwanza wa utawala wa alifungua milango ya Hekalu la BWANA, na kuikarabati. [4] Akawaingiza makuhani na Walawi ndani na kuwakutanisha katika uwanja upande wa mashariki [5] [i]na kusema: “Nisikilizeni mimi, enyi Walawi! Jitakaseni nafsi zenu sasa, mkaitakase na nyumba ya BWANA, Mungu wa baba zenu. Ondoeni uchafu wote kutoka mahali patakatifu. [6] [j]Baba zetu hawakuwa waaminifu, walifanya maovu machoni pa BWANA Mungu wetu na wakamwacha yeye. Wakageuza nyuso zao mbali na Maskani ya BWANA wakamgeuzia visogo vyao. [7] [k]Pia walifunga milango ya ukumbi wa Hekalu na kuzima taa zake. Hawakufukiza uvumba wala kutoa sadaka yoyote ya kuteketezwa katika mahali patakatifu kwa Mungu wa Israeli. [8] [l]Kwa hiyo, hasira ya BWANA ikashuka juu ya Yuda na Yerusalemu, naye akawa amewafanya kitu cha kutisha, cha kushangaza na kitu cha kufanyia mzaha kama mnavyoona kwa macho yenu wenyewe. [9] [m]Hii ndiyo sababu baba zetu wameanguka kwa upanga na ndiyo sababu wana wetu na binti zetu, pia wake zetu wamekuwa mateka. [10] [n]Sasa ninadhamiria moyoni mwangu kuweka Agano na BWANA, Mungu wa Israeli, ili hasira yake kali igeuziwe mbali nasi. [11] [o]Wanangu, basi msipuuze jambo hili sasa, kwa kuwa BWANA amewachagua ninyi msimame mbele zake na kumtumikia, mkawe watumishi wake na mkamfukizie uvumba.”

[12] [p]Ndipo Walawi wafuatao wakaanza kazi:

---

[a]**28:22** Yer 5:3; 15:7; 17:23
[b]**28:23** 2Nya 25:14; Isa 10:20; Yer 44:17-18
[c]**28:24** 2Fal 16:18; 2Nya 29:7; 30:14
[d]**28:26** 2Fal 16:19-20; 2Nya 27:7-9
[e]**28:27** Isa 14:28-32; 2Nya 21:20; 24:25
[f]**29:1** 1Nya 3:13; 2Nya 26:5; 2Fal 18:1
[g]**29:2** 2Nya 28:1; 34:2
[h]**29:3** 2Fal 18:16; 2Nya 28:24; Mit 8:17
[i]**29:5** Law 11:44; Neh 13:9; Efe 5:26-27; 1Nya 15:12; 2Nya 35:6; Eze 36:25; Mt 21:12-13; 1Kor 3:16-17; 2Kor 6:16
[j]**29:6** Eze 23:35; Dan 9:5-6; 1Nya 5:25; Eze 8:16; Yer 2:27
[k]**29:7** 2Fal 16:17-18; 2Nya 28:24
[l]**29:8** Kum 28:25; 2Nya 24:18; Law 26:32; Eze 8:16; Yer 18:16; 1Fal 9:8; Yer 19:8; 29:18
[m]**29:9** 2Nya 28:5-8, 17; Law 26:17
[n]**29:10** 2Fal 11:17; 2Nya 15:12; Neh 9:38; Ezr 10:3; 2Nya 23:16
[o]**29:11** Hes 3:6; 8:6-14; 1Nya 15:2; 1Kor 6:9
[p]**29:12** Hes 3:17-20; 2Nya 31:15

Kutoka kwa Wakohathi,
Mahathi mwana wa Amasai na
Yoeli mwana wa Azaria;
kutoka kwa Wamerari,
Kishi mwana wa Abdi na Azaria
mwana wa Yahaleleli;
kutoka kwa Wagershoni,
Yoa mwana wa Zima na Edeni
mwana wa Yoa;
13 [a]kutoka kwa wana wa Elisafani,
Shimri na Yeieli;
kutoka kwa wana wa Asafu,
Zekaria na Matania;
14 kutoka kwa wana wa Hemani,
Yehieli na Shimei;
kutoka kwa wana wa Yeduthuni,
Shemaya na Uzieli.

15 [b]Walipomaliza kuwakusanya ndugu
zao na kujiweka wakfu, wakaingia ndani
ili kutakasa Hekalu la Bwana, kama
vile mfalme alivyokuwa ameagiza, kwa
kufuata neno la Bwana. 16 [c]Makuhani
wakaingia patakatifu pa Hekalu la Bwana
ili kupatakasa. Wakatoa nje penye ua
wa Hekalu la Mungu kila kitu kichafu
walichokikuta kwenye Hekalu la Bwana.
Walawi wakavichukua na kuvipeleka nje
katika Bonde la Kidroni. 17 [d]Walianza kazi
ya utakaso siku ya kwanza ya mwezi wa
kwanza na kufikia siku ya nane ya mwezi
huo wakawa wamefikia kwenye ukumbi
wa Bwana. Kwa siku zingine nane
wakalitakasa Hekalu lenyewe la Bwana
wakakamilisha katika siku ya kumi na sita
ya mwezi huo wa kwanza.
18 Kisha wakaingia ndani kwa Mfalme
Hezekia kutoa habari na kusema:
"Tumelitakasa Hekalu lote la Bwana,
madhabahu ya sadaka ya kuteketezwa
pamoja na vyombo vyake vyote, meza ya
kupanga mikate iliyowekwa wakfu, pamoja
na vyombo vyake vyote. 19 [e]Tumeviandaa
na kuvitakasa vyombo vyote vile ambavyo
Mfalme Ahazi, kwa kukosa uaminifu kwake,
aliviondoa wakati alipokuwa mfalme. Sasa
viko mbele ya madhabahu ya Bwana."

*Ibada Hekaluni Yarejeshwa*

20 Ndipo Mfalme Hezekia akainuka
asubuhi na mapema, akakusanya pamoja
maafisa wa mji wakakwea hekaluni mwa
Bwana. 21 [f]Wakaleta mafahali saba,
kondoo dume saba, wana-kondoo dume
saba na mabeberu saba kuwa sadaka ya
dhambi kwa ajili ya ufalme, kwa ajili ya
mahali patakatifu na kwa ajili ya Yuda.
Mfalme akawaamuru makuhani, wazao
wa Aroni, kuvitoa vitu hivyo sadaka
katika madhabahu ya Bwana. 22 [g]Hivyo
wakachinja wale mafahali, nao makuhani
wakachukua ile damu na kuinyunyiza
kwenye madhabahu, halafu wakawachinja
wale kondoo dume saba na kunyunyiza
hiyo damu yao kwenye madhabahu, kisha
wakawachinja wale wana-kondoo dume na
kunyunyiza damu yao kwenye madhabahu.
23 [h]Wale mabeberu waliokuwa kwa ajili
ya sadaka ya dhambi wakaletwa mbele
ya mfalme na kusanyiko nao wakaweka
mikono yao juu hao mabeberu. 24 [i]Ndipo
makuhani wakawachinja hao mabeberu
na kuweka damu yao kwenye madhabahu
kwa ajili ya sadaka ya dhambi ili kufanya
upatanisho kwa ajili ya Israeli yote, kwa
sababu mfalme alikuwa ameamuru hiyo
sadaka ya kuteketezwa na hiyo sadaka ya
dhambi kwa ajili ya Israeli yote.
25 [j]Akawaweka Walawi kwenye Hekalu
la Bwana wakiwa na matoazi, vinubi
na zeze kama ilivyoagizwa na Daudi na
Gadi mwonaji wa mfalme pamoja na nabii
Nathani kwani hili lilikuwa limeamriwa
na Bwana kupitia manabii wake. 26 [k]Hivyo
Walawi wakasimama tayari wakiwa na ala

[a]**29:13** 1Nya 6:36
[b]**29:15** 1Nya 23:28; Isa 1:25; 2Nya 30:12
[c]**29:16** 2Sam 15:23
[d]**29:17** 1Fal 6:3
[e]**29:19** 2Nya 28:24
[f]**29:21** Law 4:13-14
[g]**29:22** Law 4:18; Hes 18:17; Ebr 9:21; Law 8:14-24
[h]**29:23** Law 4:15, 24
[i]**29:24** Kut 29:36; Law 4:20-26; Kol 1:20
[j]**29:25** 1Nya 28:19; 2Nya 8:14; 1Sam 22:5; 2Sam 24:11; 1Nya 16:4; 23:6; 25:6; 2Nya 30:12
[k]**29:26** 1Nya 15:16-24; 23:5; Hes 10:10; 2Nya 12:13; Amo 6:5; 1Nya 16:6

za uimbaji za Daudi na makuhani walikuwa
na tarumbeta zao.
27 [a]Hezekia akatoa amri ya kutoa
sadaka ya kuteketezwa madhabahuni.
Walipoanza kutoa sadaka, wakaanza pia
kumwimbia BWANA pamoja na tarumbeta
na zile ala za uimbaji za Daudi mfalme
wa Israeli. 28 Kusanyiko lote wakaabudu
kwa kusujudu, wakati waimbaji wakiwa
wanaimba na wenye tarumbeta wakipiga
tarumbeta zao. Yote haya yaliendelea
mpaka walipomaliza kutoa ile dhabihu ya
sadaka ya kuteketezwa.
29 [b]Kutoa sadaka kulipomalizika, mfalme
na kila mtu aliyekuwepo pamoja naye
wakapiga magoti na kuabudu. 30 [c]Mfalme
Hezekia na maafisa wake wakawaamuru
Walawi kumsifu BWANA kwa maneno ya
Daudi na ya Asafu mwonaji. Hivyo wakaimba
sifa kwa furaha nao wakainamisha vichwa
vyao na kuabudu.
31 [d]Kisha Hezekia akasema, "Sasa
mmejiweka wakfu kwa BWANA. Njooni
mlete dhabihu na sadaka za shukrani
Hekaluni mwa BWANA." Hivyo kusanyiko
likaleta dhabihu na sadaka za shukrani, nao
wote waliokuwa na mioyo ya hiari wakaleta
sadaka za kuteketezwa.
32 Idadi ya sadaka za kuteketezwa
zilizoletwa na kusanyiko zilikuwa mafahali
sabini, kondoo dume 100 na wana-kondoo
dume 200. Wote hawa walikuwa kwa ajili
ya sadaka za kuteketezwa kwa BWANA.
33 Wanyama waliowekwa wakfu kwa
sadaka ya kuteketezwa walikuwa mafahali
600, pamoja na kondoo na mbuzi 3,000.
34 [e]Lakini makuhani walikuwa wachache
sana kuweza kuchuna wale wanyama wote
wa sadaka za kuteketezwa, kwa hiyo ndugu
zao Walawi wakawasaidia mpaka kazi ile
ikakamilika na mpaka makuhani wengine
walipowekwa wakfu, kwa kuwa Walawi
walikuwa makini kujiweka wakfu kuliko
walivyokuwa makuhani. 35 [f]Kulikuwa na
sadaka nyingi za kuteketezwa, pamoja na
mafuta ya wanyama ya sadaka za amani na
sadaka za kinywaji ambazo ziliambatana
na sadaka za kuteketezwa.
Kwa hiyo huduma ya Hekalu la BWANA
ikarudishwa kwa upya. 36 [g]Hezekia pamoja
na watu wote wakafurahi kwa sababu ya
lile Mungu alilolifanya kwa ajili ya watu
wake, kwa kuwa lilitendeka papo hapo.

*Hezekia Aadhimisha Pasaka*

30 [h]Hezekia akatuma ujumbe kuwaita
Israeli wote na Yuda, pia akaandika
barua kwa Efraimu na Manase,
kuwakaribisha ili waje hekaluni mwa
BWANA huko Yerusalemu kuadhimisha
Pasaka kwa BWANA, Mungu wa Israeli.
2 [i]Mfalme na maafisa wake pamoja
na kusanyiko lote katika Yerusalemu
waliamua kuadhimisha Pasaka katika
mwezi wa pili. 3 [j]Kwa sababu makuhani
hawakuwa wamejitakasa idadi ya kutosha
na watu wakawa hawajakusanyika huko
Yerusalemu, hawakuwa wameweza
kuadhimisha Pasaka kwa wakati wake
wa kawaida. 4 Mpango huu ukaonekana
wafaa kwa mfalme na kusanyiko lote.
5 [k]Wakaamua kupeleka tangazo Israeli kote,
kuanzia Beer-Sheba hadi Dani, wakiwaita
watu waje Yerusalemu kuadhimisha Pasaka
ya BWANA, Mungu wa Israeli. Ilikuwa
haijaadhimishwa na idadi kubwa ya watu
kama hiyo kufuatana na yale yaliyokuwa
yameandikwa.
6 [l]Kwa amri ya mfalme, matarishi
wakapita katika Israeli na Yuda kote
wakiwa na barua kutoka kwa mfalme na
kutoka kwa maafisa wake zikisema:

"Watu wa Israeli, mrudieni BWANA,
Mungu wa Abrahamu, Isaki na Israeli,

[a]**29:27** 1Sam 16:16; 2Nya 23:18; 20:21
[b]**29:29** 2Nya 20:18; Rum 14:11
[c]**29:30** Za 32:11; Flp 4:4
[d]**29:31** Ebr 13:15-16; Kut 35:22; 25:2; Law 7:12; 2Nya 13:9
[e]**29:34** 2Nya 35:11; Hes 8:15; 2Nya 30:3; Eze 44:11; 1Nya 29:17; Za 7:10
[f]**29:35** Mwa 4:4; 35:14; Hes 15:5-10; Law 3:16; 7:11-21; Kut 29:13
[g]**29:36** Za 118:23; Mdo 2:41
[h]**30:1** Mwa 41:52; Kut 12:11; Hes 28:16
[i]**30:2** Hes 9:10
[j]**30:3** Hes 9:6-13; Kut 12:6; 2Nya 29:34
[k]**30:5** Amu 20:1
[l]**30:6** 1Sam 7:3-4; Yoe 2:13; Mal 3:7; Isa 55:6-7; Hos 6:1; 2Fal 15:19-20

ili naye awarudie ninyi mliosalia,
mlionusurika kutoka mikononi mwa
wafalme wa Ashuru. 7 [a]Msiwe kama
baba zenu na ndugu zenu, ambao
hawakuwa waaminifu kwa BWANA,
Mungu wa baba zao, hivyo akawafanya
kitu cha kushangaza kama mnavyoona.
8 [b]Msiwe na shingo ngumu, kama baba
zenu walivyokuwa, bali nyenyekeeni
kwa BWANA. Njooni mahali patakatifu,
alipopatakasa milele. Mtumikieni
BWANA Mungu wenu, ili hasira yake
kali igeuziwe mbali nanyi. 9 [c]Kama
mkimrudia BWANA ndipo wale ndugu
zenu waliotekwa pamoja na watoto
wenu watakapoonewa huruma na wale
waliowateka na kuwaachia warudi
katika nchi hii, kwa kuwa BWANA
Mungu wenu ni mwenye neema na
huruma, hatageuzia uso wake mbali
nanyi kama ninyi mkimrudia yeye."

10 [d]Matarishi wakaenda mji hadi mji
katika Efraimu na Manase, wakafika mpaka
Zabuloni, lakini watu wakawadharau
na kuwadhihaki. 11 [e]Lakini, baadhi ya
watu wa Asheri, Manase na Zabuloni,
wakajinyenyekeza wakaja Yerusalemu.
12 [f]Pia katika Yuda mkono wa Mungu
ulikuwa juu ya watu kuwapa umoja katika
kutenda yale ambayo mfalme na maafisa
wake waliwaamuru, kulingana na neno la
BWANA.

13 [g]Basi umati mkubwa wa watu
ukakusanyika huko Yerusalemu
kuadhimisha Sikukuu ya Mikate Isiyotiwa
Chachu katika mwezi wa pili. 14 [h]Wakajitia
kazini kuyaondoa yale madhabahu
yaliyokuwa huko Yerusalemu, wakayaondoa
pia yale madhabahu ya kufukizia uvumba
kwa miungu na kuyatupa Bonde la Kidroni.

15 [i]Kisha wakamchinja mwana-kondoo
wa Pasaka katika siku ya kumi na nne
ya mwezi wa pili. Makuhani na Walawi
waliona aibu, wakajitakasa na kuleta sadaka
za kuteketezwa katika Hekalu la BWANA.
16 [j]Kisha wakachukua nafasi zao za kawaida
kama ilivyoelezwa katika Sheria ya Mose
mtu wa Mungu. Makuhani wakanyunyiza
ile damu waliyokabidhiwa na Walawi.
17 [k]Kwa kuwa wengi waliokuwa katika
lile kusanyiko walikuwa hawajajitakasa,
iliwapasa Walawi wachinje wana-
kondoo wengine wa Pasaka kwa ajili ya
wale watu ambao hawakuwa safi, kwa
kufuata taratibu za ibada ili kuwatakasa
kwa BWANA. 18 [l]Ingawa watu wengi
miongoni mwa wale waliotoka Efraimu,
Manase, Isakari na Zabuloni walikuwa
hawajajitakasa, hata hivyo walikula Pasaka
kinyume na ilivyoandikwa. Lakini Hezekia
akawaombea, akisema, "BWANA, ambaye ni
mwema na amsamehe kila mmoja 19 [m]ambaye
anauelekeza moyo wake kumtafuta Mungu,
BWANA, Mungu wa baba zake, hata kama
yeye si safi kulingana na sheria za mahali
patakatifu." 20 [n]Naye BWANA akamsikia
Hezekia akawaponya watu.

21 [o]Waisraeli waliokuwa Yerusalemu
wakaadhimisha Sikukuu ya Mikate
Isiyotiwa Chachu kwa muda wa siku
saba, nao Walawi na makuhani walikuwa
wakiimba kila siku, wakiwa na ala za
uimbaji za kumsifu BWANA.

22 [p]Hezekia akazungumza akiwatia moyo
Walawi wote, ambao walionyesha ustadi
katika kumtumikia BWANA. Hivyo watu
wakala chakula cha sikukuu kwa siku saba,

---

[a]**30:7** Yer 11:10; Eze 20:18; Kum 28:25; 2Nya 29:8-10
[b]**30:8** Kut 32:9; Hes 25:4; 2Nya 29:10; Kum 10:16
[c]**30:9** Yer 25:5; Kut 3:21; 34:6-7; Mik 7:18; Law 26:40; Isa 55:7
[d]**30:10** Neh 2:19; 2Nya 36:16; Lk 8:53; Mt 21:35; Mdo 17:32; Yer 5:12; Ebr 11:36
[e]**30:11** 2Nya 11:16
[f]**30:12** Ebr 13:21; Yer 32:39; 2Nya 20:33
[g]**30:13** Hes 28:16
[h]**30:14** 2Nya 28:24; 2Sam 15:23; Isa 2:17-21
[i]**30:15** 2Nya 29:34
[j]**30:16** 2Nya 35:10
[k]**30:17** 2Nya 29:34
[l]**30:18** Kut 12:43-49; Hes 9:6-16
[m]**30:19** Ezr 7:10; 2Nya 19:3; 1Nya 29:18; Ay 11:13; 2Nya 20:33
[n]**30:20** 2Nya 6:20; 7:14; Kut 15:26; Yak 5:16; Za 103:3
[o]**30:21** Kut 12:15-17; Lk 22:1-7; Kut 13:6; 1Kor 5:7-8; Law 23:6
[p]**30:22** Isa 40:2; Kum 33:10; 2Nya 17:9; 35:3; 2Tim 4:2; Ezr 10:11

wakitoa sadaka za amani na kumshukuru
Bwana, Mungu wa baba zao.
23 [a]Kisha kusanyiko lote likakubali
kuendelea na sikukuu kwa siku saba
zaidi, kwa hiyo kwa siku saba nyingine
wakaendelea kuiadhimisha kwa furaha.
24 [b]Hezekia, mfalme wa Yuda akatoa
mafahali 1,000, kondoo na mbuzi 7,000
kwa ajili ya kusanyiko, nao maafisa
wakatoa mafahali 1,000 pamoja na kondoo
na mbuzi 10,000. Idadi kubwa ya makuhani
wakajiweka wakfu. 25 [c]Kusanyiko lote la
Yuda, pamoja na makuhani na Walawi
na lile kusanyiko lote lililotoka Israeli,
pamoja na wale wageni waliotoka Israeli
na wale walioishi katika Yuda wakafurahi.
26 Kulikuwa na furaha kubwa katika
Yerusalemu, kwa sababu tangu siku za
Mfalme Solomoni mwana wa Daudi mfalme
wa Israeli halijakuwepo jambo kama hili
katika Yerusalemu. 27 [d]Ndipo makuhani na
Walawi wakasimama wakawabariki watu,
naye Mungu akawasikia, kwa sababu
maombi yao yalifika mbinguni, makao yake
matakatifu.

*Sehemu Za Ibada Za Kipagani Zaondolewa*

31 [e]Baada ya mambo haya yote
kumalizika, Waisraeli ambao
walikuwako huko wakaenda kwenye
miji ya Yuda, wakayavunja yale mawe
ya kuabudia na kuzikatakata zile nguzo
za Ashera. Wakabomoa mahali pa juu pa
kuabudia miungu pamoja na madhabahu
zake kila mahali katika Yuda na Benyamini
na katika Efraimu na Manase. Baada ya
kuviharibu hivi vyote, Waisraeli wakarudi
katika miji yao wenyewe na kwenye milki
zao.
2 [f]Hezekia akawapanga makuhani na
Walawi katika migawanyo, kila mgawanyo
kulingana na wajibu wao, kama ni makuhani
au Walawi, ili kutoa sadaka za kuteketezwa
na sadaka za amani, kuhudumu, kushukuru
na kuimba sifa katika malango ya makao ya
Bwana. 3 [g]Mfalme akatoa matoleo kutoka
mali zake mwenyewe kwa ajili ya sadaka
za kuteketezwa za asubuhi na za jioni na
sadaka za kuteketezwa kwa siku za Sabato,
kwa Sikukuu za Mwezi Mwandamo na
kwa ajili ya sikukuu zilizoamriwa kama
ilivyoandikwa katika Sheria ya Bwana.
4 [h]Akawaagiza watu wanaoishi Yerusalemu
watoe sehemu iliyo haki ya makuhani
na Walawi ili waweze kujitoa kikamilifu
kutimiza wajibu wao katika Sheria ya
Bwana. 5 [i]Mara tu baada ya kutolewa
tangazo hilo, Waisraeli wakatoa kwa
ukarimu malimbuko ya nafaka zao, divai
mpya, mafuta na asali pamoja na vyote
vilivyotoka mashambani. Wakaleta kiasi
kikubwa cha fungu la kumi la kila kitu.
6 [j]Watu wa Israeli na Yuda walioishi katika
miji ya Yuda wakaleta pia fungu la kumi la
makundi yao ya ng'ombe na makundi ya
kondoo na mbuzi pia na fungu la kumi la
vitu vitakatifu vilivyowekwa wakfu kwa
ajili ya Bwana Mungu wao na kuvikusanya
katika malundo. 7 [k]Wakaanza kufanya haya
katika mwezi wa tatu na kumaliza katika
mwezi wa saba. 8 [l]Wakati Hezekia na
maafisa wake walipokuja na kuona yale
malundo, wakamsifu Bwana na kuwabariki
watu wake Israeli.
9 Hezekia akawauliza makuhani na
Walawi kuhusu yale malundo, 10 [m]naye
Azaria aliyekuwa kuhani mkuu, kutoka
jamaa ya Sadoki, akajibu, "Tangu watu
walipoanza kuleta sadaka zao katika
Hekalu la Bwana tumekuwa na chakula

---

[a]**30:23** 1Fal 8:65; 2Nya 17:9; Isa 40:2
[b]**30:24** 1Fal 8:5; Ezr 6:17; 2Nya 35:7-8; 29:34
[c]**30:25** 2Nya 30:11, 18
[d]**30:27** Hes 6:23; Za 68:5; Isa 57:15; 66:1
[e]**31:1** 2Fal 18:4; Isa 36:7; 2Nya 13:14
[f]**31:2** 2Nya 29:9; Za 71:22; 1Nya 23:28-32; 15:2
[g]**31:3** 1Nya 29:3; Eze 45:17; Hes 28:1; 29:40
[h]**31:4** Neh 13:10-12; Mal 2:7; 1Kor 9:13; Hes 18:8
[i]**31:5** Neh 13:12; Eze 44:30; Kum 12:17; 1Kor 15:20; Kut 22:29; 23:19; Hes 18:12; Eze 20:40; Yak 1:18; Mit 3:9
[j]**31:6** Law 27:30; Neh 13:10-12; Kum 14:28; Rut 3:7
[k]**31:7** Kut 23:16
[l]**31:8** Za 144:13-15; Mwa 14:19; 2Sam 6:18; Kum 33:29; 1Fal 8:55-56; 2Nya 6:3; Za 33:12; 144:15
[m]**31:10** 2Sam 8:17; Kut 36:5; Hag 2:19; Mal 3:10-12

cha kutosha na vingi vya kuweka akiba kwa
sababu Bwana amewabariki watu wake,
hivyo tumekuwa na kiasi kingi kilichobaki.”

*Kutambuliwa Kwa Makuhani Na Walawi*

11 Hezekia akatoa agizo la kutengeneza
vyumba vya ghala katika Hekalu la Bwana
nalo hili likafanyika. 12 [a]Kisha kwa uaminifu
wakaleta sadaka zao, mafungu yao ya kumi
na vitu vilivyowekwa wakfu. Konania
Mlawi, ndiye alikuwa msimamizi wa vitu
hivi na Shimei ndugu yake ndiye alikuwa
msaidizi wake. 13 Yehieli, Azazia, Nahathi,
Asaheli, Yeremothi, Yozabadi, Elieli,
Ismakia, Mahathi na Benaya walikuwa
waangalizi chini ya Konania na Shimei
ndugu yake, waliokuwa wamewekwa na
Mfalme Hezekia na Azaria, afisa msimamizi
wa Hekalu la Mungu.
14 Kore mwana wa Imna, Mlawi,
bawabu wa Lango la Mashariki, alikuwa
msimamizi wa sadaka za hiari zilizotolewa
kwa Mungu, akiyagawanya hayo matoleo
yaliyotolewa kwa Bwana na pia zile sadaka
zilizowekwa wakfu. 15 [b]Edeni, Miniamini,
Yeshua, Shemaya, Amaria na Shekania
walimsaidia kwa uaminifu katika miji ya
makuhani, wakiwagawia makuhani wenzao
kufuatana na migawanyo yao, wazee kwa
vijana sawasawa.
16 [c]Zaidi ya hao wakawagawia wanaume
wenye umri wa miaka mitatu au zaidi
ambao majina yao yalikuwa kwenye orodha
ya vizazi, wale wote ambao wangeingia
katika Hekalu la Bwana ili kufanya kazi zao
mbalimbali za kila siku kulingana na wajibu
katika mgawanyo wao. 17 [d]Kuandikishwa
kwa makuhani kulikuwa kwa kufuata
chimbuko la nyumba za baba zao na
Walawi kuanzia umri wa miaka ishirini
au zaidi ilikuwa kufuatana na huduma
zao, kwa migawanyo yao. 18 Makuhani
waliandikishwa pamoja na watoto wao
wadogo, wake zao, watoto wao wa kiume
na wa kike, jamii yote iliandikishwa kwa
kufuata orodha ya vizazi vyao. Kwa kuwa
walikuwa waaminifu katika kujitakasa.
19 [e]Kuhusu makuhani, wazao wa Aroni
walioishi kwenye mashamba yaliyozunguka
miji yao au katika miji mingine yoyote,
watu walitajwa majina ili kumgawia kila
mwanaume miongoni mwao na kwa wote
waliokuwa katika orodha ya vizazi vya
Walawi.
20 [f]Hivi ndivyo Hezekia alivyofanya katika
Yuda yote, akifanya lile lililo jema, sawa
na la uaminifu mbele za Bwana Mungu
wake. 21 [g]Naye katika kila kitu alichofanya
katika huduma kwenye Hekalu la Mungu na
katika utii kwa sheria na amri, alimtafuta
Mungu wake na kufanya kazi kwa moyo
wake wote. Naye hivyo akafanikiwa.

*Senakeribu Aitishia Yerusalemu*

**(2 Wafalme 18:13-37; 19:14-19, 35-37; Isaya 36:1-22; 37:8-38)**

32 [h]Baada ya yale yote aliyokuwa
amefanya Hezekia kwa uaminifu
mkubwa, Senakeribu mfalme wa Ashuru
akaja na kuvamia Yuda. Akaizunguka miji
yenye ngome kwa jeshi, akifikiri kuiteka iwe
yake. 2 [i]Hezekia alipoona kuwa Senakeribu
amekuja na kwamba alikusudia kufanya
vita juu ya Yerusalemu, 3 akafanya shauri
na maafisa wake na mashujaa wake juu
ya kuzuia maji kutoka chemchemi zilizo
nje ya mji, nao wakamsaidia. 4 [j]Umati
mkubwa wa watu ukakusanyika na kuzuia
chemchemi zote na vijito vilivyotiririka
katika nchi yote, wakisema: “Kwa nini
wafalme wa Ashuru waje na kukuta
maji tele?” 5 [k]Hezekia akafanya kazi kwa
bidii kukarabati sehemu zote zilizokuwa
zimebomoka za ukuta na kujenga minara
juu yake. Akajenga ukuta mwingine nje ya

---

[a]**31:12** 2Nya 35:9; Neh 13:13
[b]**31:15** 2Nya 29:12; Yos 21:9-19
[c]**31:16** 1Nya 23:3; Ezr 3:4
[d]**31:17** 1Nya 23:24, 27
[e]**31:19** Law 25:34; 2Nya 31:12-15; Hes 35:2
[f]**31:20** 2Fal 20:3; 22:2; 1The 2:10; 1Fal 15:5; Yn 1:47
[g]**31:21** Kum 29:9; Mit 3:9; Yos 4:7; Mal 3:10; 1Tim 4:8
[h]**32:1** 2Fal 18:13-19; Isa 37:9
[i]**32:2** Isa 22:7; Yer 1:15
[j]**32:4** 2Fal 20:20; Nah 3:14
[k]**32:5** 2Nya 25:23; Isa 22:9-10; 1Fal 9:24; 2Sam 5:9; 1Nya 11:8

ule uliokuwepo na kuimarisha Milo[a] katika
Mji wa Daudi. Akatengeneza pia silaha
nyingi na ngao.
6 [b]Akaweka maafisa wa jeshi juu ya
watu, wakawakutanisha mbele yake katika
uwanja kwenye lango la mji, naye akawatia
moyo kwa maneno haya: 7 [c]"Kuweni
hodari na wenye moyo mkuu. Msiogope,
msifadhaike wala msikate tamaa kwa
sababu ya mfalme wa Ashuru na hili jeshi
kubwa lililo pamoja naye, kwa kuwa aliye
pamoja nasi ni mkuu kuliko aliye pamoja
naye. 8 [d]Kwake uko mkono wa mwili tu,
bali kwetu yuko BWANA Mungu wetu
kutusaidia na kutupigania vita vyetu." Nao
watu wakatiwa moyo kutokana na maneno
aliyowaambia Hezekia mfalme wa Yuda.
9 [e]Hatimaye Senakeribu mfalme wa
Ashuru na majeshi yake yote walipokuwa
wameuzunguka Lakishi, akawatuma
maafisa wake kwenda Yerusalemu wakiwa
na ujumbe huu kwa Hezekia mfalme
wa Yuda, na kwa watu wote wa Yuda
waliokuwako humo, kusema:

10 [f]"Hili ndilo asemalo Senakeribu
mfalme wa Ashuru: Je, mmeweka
tumaini lenu wapi, hata mnaendelea
kukaa katika Yerusalemu, hali
mmezungukwa na jeshi? 11 [g]Hezekia
asemapo, 'BWANA Mungu wetu
atatuokoa kutokana na mkono wa
mfalme wa Ashuru,' anawapotosha
ninyi, naye atawaacha mfe kwa njaa
na kiu. 12 Je, si Hezekia mwenyewe
aliyeondoa mahali pa juu pa kuabudia
miungu pamoja na madhabahu zake,
akiwaambia Yuda wa Yerusalemu, 'Ni
lazima mwabudu mbele ya madhabahu
moja na kuteketeza dhabihu juu yake'?
13 [h]"Je, hamjui yale mimi na baba
zangu tuliyoyafanya kwa mataifa yote
ya nchi zingine? Je, miungu ya mataifa
hayo iliweza kuokoa nchi zao kutoka
mkononi mwangu? 14 Ni yupi miongoni
mwa miungu yote ya mataifa haya
ambayo baba zangu waliyaangamiza
ameweza kuwaokoa watu wake
mkononi mwangu? Inawezekanaje
basi Mungu wenu kuwaokoa mkononi
mwangu? 15 [i]Sasa basi, msikubali
Hezekia awadanganye na kuwapotosha
namna hii. Msimwamini, kwa kuwa
hakuna mungu wa taifa lolote wala wa
ufalme wowote aliyeweza kuwaokoa
watu wake kutoka mkononi mwangu
au mkononi mwa baba zangu. Sembuse
huyo mungu wenu atawaokoaje kutoka
mkononi mwangu!"

16 Maafisa wa Senakeribu wakaendelea
kunena dhidi ya BWANA aliye Mungu na
dhidi ya mtumishi wake Hezekia. 17 [j]Mfalme
pia aliandika barua akimtukana BWANA,
Mungu wa Israeli na kusema haya dhidi
yake: "Kama vile miungu ya mataifa ya
nchi nyingine ilivyoshindwa kuwaokoa
watu wao mkononi mwangu, vivyo hivyo
Mungu wa Hezekia hataweza kuwaokoa
watu wake kutoka mkononi mwangu."
18 [k]Kisha wakawaita kwa Kiebrania watu
wa Yerusalemu waliokuwa juu ya ukuta
ili kuwatisha na kuwatia hofu ili waweze
kuuteka mji. 19 [l]Wakanena juu ya Mungu
wa Yerusalemu kama vile walivyonena juu
ya miungu ya mataifa mengine ya dunia
ambayo ni kazi ya mikono ya wanadamu.
20 Mfalme Hezekia na nabii Isaya mwana
wa Amozi wakalilia mbingu katika maombi
kuhusu jambo hili. 21 [m]Naye BWANA
akamtuma malaika ambaye aliangamiza
wanajeshi wote, na viongozi na maafisa

---

[a]5 Milo maana yake Boma la Ngome.
[b]**32:6** 2Nya 30:22; Isa 40:2
[c]**32:7** Kum 31:6; 1Nya 22:13; 28:10; 2Nya 20:15; Hes 14:9; 2Fal 6:16; Za 55:18
[d]**32:8** Ay 40:9; Isa 41:10-14; 52:10; 1Sam 17:45; 2Nya 13:12; 1Nya 5:22; Rum 8:31; Yer 17:5; 1Yn 4:4; Kum 20:1-4; 31:6-8; Mit 18:10; Amo 5:14
[e]**32:9** 2Fal 18:17; Yos 10:3
[f]**32:10** Eze 29:16
[g]**32:11** Isa 37:10
[h]**32:13** 2Fal 18:33-35; Za 115:4-8
[i]**32:15** Isa 37:10; Dan 3:15; Kut 5:2; Yn 19:10-11
[j]**32:17** Isa 37:14; Za 74:22; 2Fal 19:12
[k]**32:18** 2Fal 18:28
[l]**32:19** Za 115:4; Yer 1:16; Za 135:15-18; Isa 10:10; Kum 4:28; 2Fal 19:18; Yer 10:3; Hos 8:5-6
[m]**32:21** Mwa 19:13; Isa 37:38; Yer 41:2

katika kambi ya mfalme wa Ashuru. Kwa
hiyo, mfalme wa Ashuru akarudi nchini
mwake kwa aibu. Naye alipokwenda katika
hekalu la mungu wake, baadhi ya watoto
wake wakamuua kwa upanga.
22 [a]Hivyo Bwana akamwokoa Hezekia na
watu wa Yerusalemu kutoka mkononi mwa
Senakeribu mfalme wa Ashuru na kutoka
mikononi mwa wengine wote. Bwana
akawastarehesha kila upande. 23 [b]Watu
wengi wakaleta sadaka Yerusalemu kwa
ajili ya Bwana na zawadi za thamani kwa
ajili ya Hezekia mfalme wa Yuda. Tangu
hapo na kuendelea, Hezekia aliheshimiwa
sana na mataifa yote.

*Kiburi Cha Hezekia, Mafanikio Na Kifo*

**(2 Wafalme 20:1-3, 12-19; Isaya 38:1-3; 39:1-8)**

24 [c]Katika siku hizo, Hezekia akaugua,
naye akawa karibu kufa. Akamwomba
Bwana, ambaye alimjibu na kumpa
ishara. 25 [d]Lakini moyo wa Hezekia ukajaa
majivuno na hakuonyesha itikio kwa
wema aliotendewa, kwa hiyo ghadhabu
ya Bwana ikawa juu yake na juu ya Yuda
na Yerusalemu. 26 [e]Ndipo Hezekia akatubu
kwa ajili ya kiburi cha moyo wake, kama
walivyofanya watu wa Yerusalemu, kwa
hiyo ghadhabu ya Bwana haikuja juu yao
katika siku za Hezekia.
27 [f]Hezekia alikuwa na utajiri mwingi
sana na heshima, naye akajifanyia hazina
kwa ajili ya fedha yake na dhahabu na kwa
ajili ya vito vyake vya thamani, vikolezi,
ngao na aina zote za vyombo vya thamani.
28 Akajenga pia maghala ya kuhifadhi
mavuno ya nafaka, divai mpya na mafuta.
Akatengeneza mabanda kwa ajili ya aina
mbalimbali za mifugo, na mazizi kwa ajili
ya kondoo na mbuzi. 29 [g]Akajenga vijiji na
kujipatia idadi kubwa ya kondoo na mbuzi,
pamoja na ng'ombe kwa kuwa Mungu
alikuwa amempa utajiri mwingi sana.
30 [h]Ilikuwa ni Hezekia aliyeziba njia za
kutolea maji za chemchemi za juu za Gihoni
na kuyaelekeza maji kutiririkia upande wa
magharibi wa Mji wa Daudi. Akafanikiwa
katika kila kitu alichofanya. 31 [i]Lakini
wakati wajumbe walipotumwa na watawala
wa Babeli kumuuliza juu ya ishara ambayo
ilitokea katika nchi, Mungu alimwacha ili
kumjaribu na kujua kila kitu kilichokuwa
moyoni mwake.
32 [j]Matukio mengine ya utawala wa
Hezekia na matendo yake ya kujitoa kwa
moyo yameandikwa katika maono ya nabii
Isaya mwana wa Amozi kwenye kitabu cha
wafalme wa Yuda na Israeli. 33 [k]Hezekia
akalala na baba zake na akazikwa kwenye
kilima mahali yalipo makaburi ya wazao wa
Daudi. Yuda wote na watu wa Yerusalemu
wakamheshimu alipofariki. Naye Manase
mwanawe akawa mfalme baada yake.

*Manase Mfalme Wa Yuda*

**(2 Wafalme 21:1-18)**

33 [l]Manase alikuwa na umri wa miaka kumi
na miwili alipoanza kutawala, naye
akatawala huko Yerusalemu miaka hamsini
na mitano. 2 [m]Akafanya maovu machoni pa
Bwana, akafuata desturi za machukizo za
mataifa ambayo Bwana aliyafukuza mbele
ya Waisraeli. 3 [n]Akajenga upya mahali pa
juu pa kuabudia miungu ambapo Hezekia
baba yake, alikuwa amepabomoa, pia
akasimamisha madhabahu za Mabaali
na nguzo za Maashera. Akalisujudia jeshi

---

[a]**32:22** Za 18:48-50; Isa 31:5
[b]**32:23** 1Sam 10:27; Za 76:11; 1Nya 29:25; 2Nya 17:5
[c]**32:24** Isa 38:1
[d]**32:25** 2Fal 14:10; Kum 32:6; 2Nya 26:16; 19:2; 24:18; Kum 8:12; Za 116:12; Lk 17:17; 2Fal 14:10; Hab 2:4; 1Tim 3:6; 1Pet 5:5-6
[e]**32:26** Yer 26:18-19; 2Nya 34:27-28; 2Fal 19:20; Isa 39:8
[f]**32:27** 1Nya 29:12; 2Nya 9:24
[g]**32:29** 2Nya 29:12
[h]**32:30** 2Fal 18:17; 1Fal 1:33; Isa 22:9
[i]**32:31** Isa 13:1; 39:1; 38:7; Kum 8:16; Mwa 22:1; Yn 1:12
[j]**32:32** Isa 36:1; 2Fal 18:1
[k]**32:33** 1Sam 2:30; Mit 10:7
[l]**33:1** 2Fal 21:1; 1Nya 3:13
[m]**33:2** Yer 15:4; Kum 18:9; Law 18:24-30; 2Nya 28:3; 2Fal 17:11-15
[n]**33:3** Kum 16:21-22; 2Nya 24:18; 2Fal 23:5-11; Kum 17:3; 2Nya 30:14; 2Fal 18:4; Yer 8:2; Sef 1:2

lote la angani na kuliabudu. 4 [a]Akajenga
madhabahu katika Hekalu la BWANA
ambamo BWANA alikuwa amesema, “Jina
langu litadumu Yerusalemu milele.”
5 [b]Katika nyua zote mbili za Hekalu la
BWANA akajenga madhabahu kwa ajili ya
jeshi lote la angani. 6 [cd]Akawatoa wanawe
kuwa kafara kwa kuwapitisha katika moto
katika Bonde la Ben-Hinomu, akafanya
ulozi, uaguzi na uchawi, akataka ushauri
kwa wenye pepo wa utambuzi na wenye
kuwasiliana na mizimu. Akafanya maovu
mengi machoni pa BWANA, akaichochea
hasira yake.
7 [e]Akachukua ile sanamu aliyoichonga na
kuiweka katika Hekalu la Mungu ambalo
Mungu alikuwa amemwambia Daudi na
mwanawe Solomoni, “Katika Hekalu hili
na katika Yerusalemu niliouchagua kutoka
kabila zote za Israeli, nitaliweka Jina langu
milele. 8 [f]Sitaifanya tena miguu ya Waisraeli
iondoke tena katika nchi niliyowapa
baba zenu, ikiwa watakuwa waangalifu
kufanya kila kitu nilichowaamuru kuhusu
sheria zote, maagizo na amri zilizotolewa
kwa mkono wa Mose.” 9 [g]Lakini Manase
akawaongoza Yuda na watu wa Yerusalemu
katika upotovu, kiasi kwamba walifanya
maovu mengi kuliko mataifa ambayo
BWANA aliwaangamiza mbele ya Waisraeli.
10 [h]BWANA akasema na Manase pamoja na
watu wake, lakini hawakumjali. 11 [i]Hivyo
BWANA akaleta juu yao majemadari wa jeshi
la mfalme wa Ashuru, ambao walimchukua
Manase kwenda kifungoni, wakaweka
ndoana katika pua yake, wakamfunga
kwa pingu za shaba na kumpeleka Babeli.
12 [j]Katika dhiki yake akamsihi BWANA
Mungu wake na kujinyenyekeza sana
mbele za Mungu wa baba zake. 13 [k]Naye
alipomwomba, BWANA akaguswa na kule
kusihi kwake na akasikiliza kilio chake, kwa
hiyo akamrudisha Yerusalemu na kwenye
ufalme wake. Ndipo Manase akatambua
kwamba BWANA ndiye Mungu.
14 [l]Baadaye akajenga ukuta wa nje wa Mji
wa Daudi, magharibi mwa chemchemi ya
Gihoni katika bonde, hadi kufikia ingilio la
Lango la Samaki na akakizunguka kilima
cha Ofeli, pia akaufanya kuwa mrefu zaidi.
Akawaweka majemadari katika miji yote ya
Yuda iliyokuwa imejengewa ngome.
15 [m]Akaondolea mbali miungu ya kigeni na
kuondoa sanamu kutoka Hekalu la BWANA
pamoja na madhabahu zote alizozijenga
katika kile kilima kilichojengwa Hekalu na
katika Yerusalemu, akazitupa nje ya mji.
16 [n]Kisha akarudisha madhabahu ya BWANA
na kutolea juu yake dhabihu za sadaka za
amani pamoja na sadaka za shukrani, naye
akawaamuru Yuda wamtumikie BWANA,
Mungu wa Israeli. 17 [o]Lakini hata hivyo
watu wakaendelea kutoa dhabihu mahali pa
juu pa kuabudia miungu, lakini wakimtolea
BWANA Mungu wao peke yake.
18 Matukio mengine ya utawala wa
Manase, maombi yake kwa Mungu wake
na maneno aliyoambiwa na waonaji
walionena naye kwa jina la BWANA, Mungu
wa Israeli, yameandikwa katika kitabu
cha kumbukumbu za wafalme wa Israeli.
19 [p]Maombi yake, pamoja na jinsi Mungu
alivyoguswa na kusihi kwake, pia dhambi
zake zote na kukosa kwake uaminifu
pamoja na sehemu alizojenga mahali pa

[a]**33:4** 2Nya 7:16; 1Fal 8:29; Kum 12:11
[b]**33:5** 2Nya 4:9
[c]**33:6** Law 18:21; Kum 18:10; Kut 22:18; Law 19:31; 1Sam 28:13
[d]**33:6** 2Nya 28:3; Eze 23:37; 2Fal 21:6
[e]**33:7** 2Nya 7:16; Za 132:14
[f]**33:8** 2Sam 7:10
[g]**33:9** Yer 15:4; Eze 5:7
[h]**33:10** Neh 9:29; Yer 25:4
[i]**33:11** Kum 28:36; Ay 36:8; Za 107:10-11
[j]**33:12** 2Nya 32:26; 1Pet 5:6; Yer 31:18-20; Lk 15:16-18; Kum 4:30-31; Za 118:5; Hos 5:15; Yn 2:2; Mik 6:9; Kut 10:3; Lk 18:4; 2Nya 32:16
[k]**33:13** 1Nya 5:20; Ezr 8:23; Mao 3:55-56; Za 142:1-7; 9:16; Dan 4:25
[l]**33:14** 1Fal 1:33; Neh 3:3; 2Nya 27:3; Neh 3:26
[m]**33:15** 2Fal 23:12
[n]**33:16** Law 7:11-18
[o]**33:17** 1Fal 22:43; 2Nya 32:12; 2Fal 15:4; 2Nya 15:17
[p]**33:19** 2Nya 6:37; 2Fal 21; 17

juu pa kuabudia miungu, kule kusimamisha
nguzo za Ashera na sanamu kabla ya
kujinyenyekeza kwake, yote yameandikwa
katika kumbukumbu za waonaji. 20 [a]Manase
akalala pamoja na baba zake akazikwa
katika jumba lake la kifalme. Naye Amoni
mwanawe akawa mfalme baada yake.

*Amoni Mfalme Wa Yuda*

**(2 Wafalme 21:19-26)**

21 Amoni alikuwa na miaka ishirini na
miwili, alipoanza kutawala, naye akatawala
huko Yerusalemu kwa miaka miwili.
22 Akatenda maovu machoni mwa Bwana,
kama baba yake Manase alivyofanya.
Amoni akaabudu na kutoa dhabihu kwa
sanamu zote alizokuwa ametengeneza
Manase. 23 [b]Lakini tofauti na Manase baba
yake, hakujinyenyekeza mbele za Bwana,
badala yake Amoni aliongeza hatia zaidi
na zaidi.

24 [c]Watumishi wa Amoni wakafanya fitina
juu yake, nao wakamuulia kwake nyumbani.
25 [d]Kisha watu wa nchi wakawaua wale wote
waliokuwa wamefanya hila dhidi ya Mfalme
Amoni. Wakamfanya Yosia mwanawe kuwa
mfalme mahali pake.

*Yosia Afanya Matengenezo*

**(2 Wafalme 22:1-2)**

34 [e]Yosia alikuwa na miaka minane
alipoanza kutawala, naye akatawala
huko Yerusalemu miaka thelathini na
mmoja. 2 [f]Akafanya yaliyo mema machoni
pa Bwana na kuenenda katika njia za
Daudi baba yake, hakugeuka upande wa
kuume wala wa kushoto.

3 [g]Katika mwaka wa nane wa utawala
wake, alipokuwa angali bado mdogo,
alianza kumtafuta Mungu wa Daudi baba
yake. Katika mwaka wake wa kumi na
mbili alianza kusafisha mahali pa juu pa
kuabudia miungu pa Yuda na Yerusalemu,
akiondoa nguzo za Ashera, sanamu za
kuchonga na vinyago vya kusubu. 4 [h]Mbele
ya macho yake, wakazibomoa madhabahu
za Mabaali, wakazivunja madhabahu za
kufukizia uvumba zilizokuwa zimesimama
juu yake, wakazivunja nguzo za Ashera,
sanamu na vinyago. Hivi alivivunja vipande
vipande na kuvisambaza juu ya makaburi
ya waliokuwa wamevitolea kafara.
5 [i]Akachoma mifupa ya makuhani wao
juu ya madhabahu zao na kwa njia hiyo
akaitakasa Yuda na Yerusalemu. 6 Katika
miji ya Manase, Efraimu na Simeoni, hadi
Naftali na kwenye magofu yanayoizunguka,
7 [j]akavunja madhabahu na nguzo za Ashera
na kuzipondaponda hizo sanamu hadi
zikawa unga na kukata vipande vipande
madhabahu zote za kufukizia uvumba katika
Israeli yote. Kisha akarudi Yerusalemu.

8 [k]Katika mwaka wa kumi na nane wa
utawala wa Yosia, ili kutakasa nchi na
Hekalu, akawatuma Shafani, mwana wa
Azalia na Maaseya mtawala wa mji, pamoja
na Yoa mwana wa Yoahazi, mwandishi ili
kukarabati Hekalu la Bwana Mungu wake.

9 [l]Wakamwendea Hilkia kuhani
mkuu na kumpa fedha ambazo zilikuwa
zimeletwa ndani ya Hekalu la Bwana
ambazo Walawi waliokuwa mabawabu
walikuwa wamezikusanya kutoka kwa
watu wa Manase, Efraimu na mabaki
wote wa Israeli kutoka kwa watu wote
wa Yuda na Benyamini na wakazi wa
Yerusalemu. 10 Kisha wakazikabidhi hizo
fedha kwa watu waliowekwa ili kusimamia
kazi ya Hekalu la Bwana. Hawa watu
waliwalipa wafanyakazi waliokarabati na
kutengeneza Hekalu lipate kurudi katika

---

[a]**33:20** 2Fal 21:18-20
[b]**33:23** Kut 10:3; 2Nya 7:14; Za 18:27; 147:6; Mit 3:34
[c]**33:24** 2Nya 24:25
[d]**33:25** 2Nya 22:1; 2Fal 21:23-24; 2Nya 25:27-28
[e]**34:1** 1Nya 3:14; Sef 1:1; 1Fal 3:7-9; 13:2; 2Nya 35:25
[f]**34:2** 2Nya 29:2
[g]**34:3** 1Fal 13:2; 1Sam 1:24; 1Nya 16:11; Mit 8:17; Za 119:9; 2Tim 3:15; 2Nya 15:2; 1Fal 13:2
[h]**34:4** Kut 34:13; 2Fal 23:11; Mik 1:5; Kut 32:30; Law 26:30
[i]**34:5** 1Fal 13:2
[j]**34:7** Kut 32:20; Kum 9:21; 2Nya 31:1
[k]**34:8** 2Fal 22:3
[l]**34:9** 1Nya 6:13; 2Nya 35:8; 2Fal 12:4

hali yake. 11 [a]Wakawapa pia mafundi
seremala na waashi fedha ili kununua mawe
yaliyochongwa, mbao kwa ajili ya kufungia
na boriti kwa ajili ya majengo ambayo
wafalme wa Yuda walikuwa wameyaacha
yakawa magofu.
12 [b]Watu wakafanya kazi kwa uaminifu.
Waliokuwa wamewekwa juu yao ili
kuwaelekeza ni Yahathi na Obadia, Walawi
wa uzao wa Merari, Zekaria na Meshulamu,
waliotoka kwenye uzao wa Kohathi. Walawi
wote waliokuwa na ufundi wa kupiga ala za
uimbaji, 13 [c]wakawa wasimamizi wa vibarua
na kuwaongoza wale waliofanya kila aina
ya kazi. Baadhi ya Walawi walikuwa
waandishi, maafisa na mabawabu.

*Kitabu Cha Sheria Chapatikana*

**(2 Wafalme 22:3-20)**

14 [d]Wakati walikuwa wakizitoa nje fedha
zilizokuwa zimetolewa kwenye Hekalu
la BWANA, kuhani Hilkia akakipata kile
Kitabu cha Sheria ya BWANA kilichokua
kimetolewa kwa mkono wa Mose.
15 [e]Hilkia akamwambia Shafani mwandishi,
"Nimekipata Kitabu cha Sheria ndani ya
Hekalu la BWANA." Akampa Shafani kile
Kitabu.
16 Kisha Shafani akakipeleka kile
Kitabu kwa mfalme na kumwambia,
"Maafisa wako wanafanya kila kitu kama
walivyokabidhiwa kufanya. 17 Wamelipa
fedha zilizokuwa katika Hekalu la BWANA
na wamewakabidhi wasimamizi na
wafanyakazi." 18 [f]Kisha Shafani mwandishi
akamwarifu mfalme kuwa, "Kuhani Hilkia
amenipa Kitabu." Naye Shafani akakisoma
mbele ya mfalme.
19 [g]Mfalme aliposikia yale maneno ya
Sheria, akayararua mavazi yake. 20 [h]Akatoa
maagizo haya kwa Hilkia, Ahikamu mwana
wa Shafani, Abdoni mwana wa Mika,
Shafani mwandishi na Asaya mtumishi
wa mfalme, 21 [i]"Nendeni mkamuulize
BWANA kwa ajili yangu na kwa ajili ya
mabaki walioko Israeli na Yuda kuhusu
yale yaliyoandikwa ndani ya kitabu hiki
ambacho kimepatikana. Hasira ya BWANA
ni kubwa mno ambayo imemwagwa juu
yetu kwa sababu baba zetu hawakulishika
neno la BWANA wala hawajatenda kulingana
na yale yote yaliyoandikwa katika Kitabu
hiki."
22 [j]Hilkia pamoja na wale wote mfalme
aliokuwa amewatuma pamoja naye
wakaenda kuzungumza na nabii mke
aitwaye Hulda, aliyekuwa mke wa Shalumu
mwana wa Tokhathi, mwana wa Hasra
mtunzaji wa chumba cha mavazi. Hulda
aliishi Yerusalemu, katika Mtaa wa Pili.
23 Akawaambia, "Hivi ndivyo asemavyo
Bwana, Mungu wa Israeli: Mwambieni yule
mtu aliyewatuma ninyi kwangu, 24 [k]'Hivi
ndivyo asemavyo Bwana: Nitaleta maafa
juu ya mahali hapa na watu wake, laana
zote zilizoandikwa ndani ya hicho kitabu
ambazo zimesomwa mbele ya mfalme wa
Yuda. 25 [l]Kwa sababu wameniacha mimi na
kufukiza uvumba kwa miungu mingine na
kunighadhibisha kwa kazi yote ya mikono
yao, hivyo hasira yangu itamwagwa
juu ya mahali hapa, wala haitatulizwa.'
26 Mwambieni mfalme wa Yuda, ambaye
amewatuma kumuuliza BWANA, 'Hivi
ndivyo asemavyo BWANA, Mungu wa
Israeli kuhusu maneno uliyoyasikia: 27 [m]Kwa
kuwa moyo wako ulikuwa msikivu na
ulijinyenyekeza mbele za Mungu uliposikia
kile nilichosema dhidi ya mahali hapa na
watu wake na kwa sababu ulijinyenyekeza

[a]**34:11** 2Nya 24:12; 33:4-7
[b]**34:12** 2Nya 12:15; 1Nya 25:1; Neh 7:2; 1Kor 4:2; 2Fal 12:15; 22:7; Mt 28:20
[c]**34:13** 1Nya 23:4; Ezr 7:6; Yer 8:8; Mt 26:3
[d]**34:14** Kum 31:24-26; 2Fal 22:8
[e]**34:15** 2Fal 22:8; Neh 8:1
[f]**34:18** Kum 17:19; Yos 1:8
[g]**34:19** Kum 28:3-68; Yos 7:6; Gal 2:19; 3:10-11; Rum 7:7-14; Hab 3:16; Rum 3:20; 2Fal 19:1; Neh 8:9; Za 94:12-13; 119:120; Yer 23:9; Yoe 2:13
[h]**34:20** 2Fal 22:3-12
[i]**34:21** Mao 2:4; 4:11; Eze 36:18; 2Fal 17:6
[j]**34:22** Kut 15:20; Lk 2:36; Mdo 21:9; Neh 6:14; Amu 4:4; 2Fal 22:14
[k]**34:24** Mit 16:4; 2Nya 36:14-20; Kum 28:15-68; Dan 9:11-16; Yos 23:16; 2Fal 21:12; 23:26-27; Isa 5:5; Yer 25:9; Amo 3:6; Zek 1:6
[l]**34:25** 2Nya 33:3-6; Yer 22:9
[m]**34:27** 2Nya 12:7; 32:26; Za 86:5

mbele zangu na uliyararua mavazi yako
na kulia mbele zangu, nimekusikia, asema
BWANA. 28 [a]Basi nitakukusanya kwa baba
zako, nawe utazikwa kwa amani. Macho
yako hayataona maafa yote nitakayoleta juu
ya mahali hapa na juu ya wote wanaoishi
hapa.' "

Kwa hiyo wakampelekea mfalme jibu
lake.

*Yosia Afanya Agano La Kutii*

**(2 Wafalme 23:1-20)**

29 [b]Kisha mfalme akawaita pamoja wazee
wote wa Yuda na Yerusalemu. 30 Akapanda
kwenda hekaluni mwa BWANA pamoja
na watu wa Yuda, watu wa Yerusalemu,
makuhani na Walawi, watu wote, wakubwa
kwa wadogo. Akasoma wakiwa wanasikia
maneno yote ya Kitabu cha Agano, ambacho
kilikuwa kimepatikana katika Hekalu la
BWANA. 31 [c]Mfalme akasimama karibu
na nguzo yake na kufanya upya Agano
mbele za BWANA ili kumfuata BWANA na
kuzishika amri zake, maagizo na sheria kwa
moyo wake wote na kwa roho yake yote na
ili kuyatii maneno ya Agano yaliyoandikwa
katika kitabu hiki.

32 [d]Ndipo akamtaka kila mmoja katika
Yerusalemu na Benyamini kuweka ahadi
zao wenyewe kwa hilo Agano, watu wa
Yerusalemu wakafanya hivyo kwa kufuata
Agano la BWANA, Mungu wa baba zao.

33 [e]Yosia akaondoa machukizo yote ya
sanamu kutoka nchi yote iliyokuwa mali
ya Waisraeli na akawataka wale wote
waliokuwako katika Israeli wamtumikie
BWANA Mungu wao. Kwa muda wote
alioishi, hawakushindwa kumfuata BWANA,
Mungu wa baba zao.

*Mfalme Yosia Anaadhimisha Pasaka*

**(2 Wafalme 23:21-23)**

35 [f]Yosia akaadhimisha Pasaka kwa
BWANA katika Yerusalemu, mwana-
kondoo wa Pasaka akachinjwa siku ya kumi
na nne ya mwezi wa kwanza. 2 [g]Akawaweka
makuhani kwenye wajibu wao na kuwatia
moyo katika utumishi wa Hekalu la BWANA.
3 [h]Akawaambia Walawi, waliowafundisha
Waisraeli wote na waliokuwa wamejiweka
wakfu kwa ajili ya kazi ya BWANA,
"Liwekeni hilo Sanduku takatifu katika
Hekalu lile alilojenga Solomoni mwana
wa Daudi mfalme wa Israeli. Halipaswi
kubebwa huku na huko mabegani mwenu.
Sasa mtumikieni BWANA Mungu wenu
na watu wake Israeli. 4 [i]Jiandaeni kwa
kufuata jamaa zenu katika migawanyo
yenu, kufuatana na maelezo yaliyoandikwa
na Daudi mfalme wa Israeli na mwanawe
Solomoni.

5 "Simameni mahali patakatifu kwa
kufuata migawanyo ya jamaa za baba zenu
kulingana na koo zenu na pawepo Walawi
kwa ajili ya kila mgawanyo wa nyumba
ya baba zenu. 6 [j]Chinjeni mwana-kondoo
wa Pasaka, jitakaseni, nanyi kwa niaba ya
koo zenu fanyeni maandalizi, mkitenda
sawasawa na neno la BWANA kwa mkono
wa Mose."

7 [k]Ndipo Yosia akawapa watu wote wana-
mbuzi waliokuwepo jumla ya kondoo
wapatao 30,000 kwa ajili ya sadaka ya
Pasaka, pia na ng'ombe 10,000, vyote hivi
kutoka mali binafsi ya mfalme.

8 [l]Pia maafisa wake, wakatoa kwa hiari
yao wakawapa watu, makuhani na Walawi.
Hilkia, Zekaria na Yehieli, waliokuwa
maafisa wakuu wa Hekalu la Mungu,

[a]**34:28** 2Nya 35:20-25; 32:26
[b]**34:29** 2Fal 23:1
[c]**34:31** 1Fal 7:15; 2Fal 11:14-17; 2Nya 29:10; Kum 13:4
[d]**34:32** Yer 3:10; 2Nya 14:2
[e]**34:33** 1Fal 11:5; Yer 3:10; 2Nya 24:2

[f]**35:1** Kut 12:1-30; Hes 9:3; Eze 45:21; Ezr 6:17; 2Fal 23:21
[g]**35:2** Ezr 6:18-19; 2Nya 23:18; 29:11
[h]**35:3** Kum 33:10; 1Nya 23:26; 2Nya 34:14; 30:22; 5:7
[i]**35:4** 1Nya 9:10-13; Ezr 6:15; 2Nya 8:14
[j]**35:6** Law 11:44; 2Nya 29:5-15; Kut 19:10; Ebr 9:13-14; Kut 19:10; Ezr 6:20; Za 51:7; Yoe 2:16; 2Nya 30:3, 15
[k]**35:7** 2Nya 30:24; Mik 6:7; 2Nya 31:3
[l]**35:8** 1Nya 29:3; 6:13; 2Kor 9:7

wakawapa makuhani sadaka za Pasaka
wana-kondoo na wana-mbuzi 2,600 na
mafahali 300. [9] [a]Konania na nduguze
wawili, Shemaya na Nethaneli, pamoja na
Hashabia, Yeieli na Yozabadi waliokuwa
viongozi wa Walawi, nao pia wakawapa
Walawi wana-kondoo na wana-mbuzi 5,000
na mafahali 500, kwa ajili ya sadaka za
Pasaka.

[10] [b]Huduma ilipomalizika kuandaliwa
makuhani wakasimama mahali pao na
Walawi katika migawanyo yao kama
mfalme alivyokuwa ameamuru. [11] [c]Wana-
kondoo wa Pasaka wakachinjwa, nao
makuhani wakanyunyiza ile damu
waliyokabidhiwa, wakati Walawi wakiwa
wanawachuna wale wanyama ngozi.
[12] [d]Wakatenga sadaka za kuteketezwa
ili waweze kugawia ili migawanyo kwa
kufuata jamaa za baba zao ili watoe
sadaka kwa BWANA kama ilivyoandikwa
katika Kitabu cha Mose. Wakafanya vivyo
hivyo kwa wale mafahali. [13] [e]Wakawaoka
wale wanyama wa Pasaka kwenye moto
kama ilivyoamriwa, wakachemsha zile
sadaka takatifu kwenye vyungu, masufuria
makubwa na vikaango na kuwagawia
watu wote upesi. [14] [f]Hatimaye wakafanya
maandalizi kwa ajili yao wenyewe na
kwa ajili ya makuhani, kwa sababu
wale makuhani, yaani, wazao wa Aroni,
walikuwa wanatoa sadaka za kuteketezwa
pamoja na zile sehemu zilizonona mpaka
usiku. Hivyo Walawi wakafanya maandalizi
kwa ajili yao wenyewe na kwa ajili ya
makuhani wa uzao wa Aroni.

[15] [g]Waimbaji, wazao wa Asafu, walikuwa
katika nafasi zao, kama ilivyoagizwa na
Mfalme Daudi, Asafu, Hemani na Yeduthuni
mwonaji wa Mfalme. Mabawabu katika
kila lango hawakuhitaji kuacha nafasi zao
kwa sababu Walawi wenzao walifanya
maandalizi kwa ajili yao.

[16] [h]Kwa hiyo wakati ule huduma yote
ya BWANA ilifanyika katika kuadhimisha
Pasaka, kutoa sadaka za kuteketezwa juu ya
madhabahu ya BWANA kama alivyoamuru
Mfalme Yosia. [17] [i]Waisraeli waliokuwepo
wakaadhimisha Pasaka wakati huo na
Sikukuu ya Mikate Isiyotiwa Chachu kwa
siku saba. [18] [j]Kulikuwa hakujafanyika
Pasaka kama hii katika Israeli tangu siku
za nabii Samweli wala hakukuwa na
mfalme yeyote wa Israeli ambaye kamwe
alishaadhimisha Pasaka kama ile aliyofanya
Mfalme Yosia, akiwa na makuhani, Walawi
na watu wote wa Yuda na watu wa Israeli
waliokuwepo huko, pamoja na watu wa
Yerusalemu. [19] Pasaka iliadhimishwa katika
mwaka wa kumi na nane wa utawala wa
Mfalme Yosia.

*Kifo Cha Yosia*

**(2 Wafalme 23:28-30)**

[20] [k]Baada ya haya yote, Yosia alipomaliza
kulitengeneza vizuri Hekalu, Neko mfalme
wa Misri, akapanda ili kupigana huko
Karkemishi katika Mto Frati, naye Yosia
akatoka kwenda kupigana naye. [21] [l]Lakini
Neko akamtumia wajumbe kusema,
"Kuna ugomvi gani kati yangu mimi na
wewe, Ee Mfalme wa Yuda? Si wewe
ninayekushambulia wakati huu, bali ile
nyumba ambayo nina vita nayo, Mungu
ameniambia niharakishe, kwa hivyo acha
kumpinga Mungu, ambaye yuko pamoja
nami, la sivyo atakuangamiza."

[22] [m]Lakini hata hivyo, Yosia hakukubali
kumwacha, bali alijibadilisha ili kupigana
naye vita. Hakusikiliza yale Neko aliyokuwa
amemwambia kwa agizo la Mungu bali

---

[a]**35:9** 2Nya 31:12-13
[b]**35:10** Ezr 6:18; 2Nya 30:16
[c]**35:11** 2Nya 29:22; 30:17
[d]**35:12** Law 3:3
[e]**35:13** Law 6:25; 1Sam 2:13-15; Kut 12:8; 13:6; Law 23:5-6; 2Nya 30:21; 1Kor 5:7-8
[f]**35:14** Kut 29:13
[g]**35:15** Neh 12:46; Za 68:25
[h]**35:16** 2Nya 3:10; Za 35:16; Yer 5:12; 32:3
[i]**35:17** Kut 12:15; Hes 28:16-17; Kum 16:3-8
[j]**35:18** 2Fal 23:22-23
[k]**35:20** Isa 10:9; Yer 46:2; Mwa 2:14; 2Fal 23:29; 25:11
[l]**35:21** 2Fal 18:25; Dan 4:35; 1Fal 13:18; Isa 36:10; Yer 25:9
[m]**35:22** Amu 5:19; 1Sam 28:8; 1Fal 22:30; 14:2; 2Nya 18:29

alikwenda kupigana naye katika tambarare
ya Megido.
23 [a]Wapiga upinde wakampiga Mfalme
Yosia, naye akawaambia maafisa wake,
“Niondoeni, nimejeruhiwa vibaya sana.”
24 [b]Kwa hiyo wakamshusha kutoka kwenye
gari lake la farasi, wakamweka kwenye
gari lingine alilokuwa nalo na kumleta
Yerusalemu, ambako alifia. Akazikwa
katika makaburi ya baba zake, nayo Yuda
yote na Yerusalemu wakamwombolezea
Yosia.
25 [c]Nabii Yeremia akatunga maombolezo
kwa ajili ya kifo chake, nao waimbaji
wote, wanaume kwa wanawake, hufanya
ukumbusho wa Yosia katika maombolezo
hadi leo. Haya yakafanywa desturi
katika Israeli, nayo yameandikwa katika
Maombolezo.
26 [d]Matukio mengine ya utawala wa Yosia
na matendo yake mema, kulingana na yale
yaliyoandikwa katika sheria ya Bwana:
27 matukio yote, kuanzia mwanzo hadi
mwisho, yameandikwa katika kitabu cha
wafalme wa Israeli na Yuda.

*Mfalme Yehoahazi Wa Yuda*

### (2 Wafalme 23:30-35)

36 [e]Watu wa nchi wakamchukua
Yehoahazi mwana wa Yosia na
kumfanya mfalme mahali pa baba yake
huko Yerusalemu.
2 Yehoahazi alikuwa na umri wa miaka
ishirini na mitatu alipoanza kutawala,
akatawala huko Yerusalemu kwa miezi
mitatu. 3 Mfalme wa Misri akamwondoa
madarakani huko Yerusalemu na akatoza
Yuda kodi ya talanta 100[f] za fedha na
talanta moja[g] ya dhahabu. 4 [h]Mfalme
wa Misri akamweka Eliakimu, nduguye
Yehoahazi, kuwa mfalme juu ya Yuda
na Yerusalemu na kubadili jina la
Eliakimu kuwa Yehoyakimu. Lakini Neko
akamchukua Yehoahazi, Nduguye Eliakimu
akampeleka Misri.

*Yehoyakimu Mfalme Wa Yuda*

### (2 Wafalme 23:35–24:7)

5 [i]Yehoyakimu alikuwa na umri wa miaka
ishirini na mitano alipoanza kutawala, naye
akatawala huko Yerusalemu miaka kumi
na mmoja. Akafanya maovu machoni pa
Bwana Mungu wake. 6 [j]Nebukadneza
mfalme wa Babeli akamshambulia na
kumfunga kwa pingu za shaba akampeleka
Babeli. 7 [k]Nebukadneza akachukua pia
vyombo kutoka Hekalu la Bwana na
kuviweka katika hekalu lake[l] huko Babeli.
8 [m]Matukio mengine ya utawala wa
Yehoyakimu, machukizo aliyoyafanya
na yote yaliyoonekana dhidi yake,
yameandikwa katika kitabu cha wafalme
wa Israeli na Yuda. Naye Yehoyakini
mwanawe akawa mfalme baada yake.

*Yehoyakini Mfalme Wa Yuda*

### (2 Wafalme 24:8-17)

9 [n]Yehoyakini alikuwa na miaka kumi
na minane alipoanza kutawala, naye
akatawala huko Yerusalemu miezi mitatu
na siku kumi. Akafanya yaliyo maovu
machoni pa Bwana. 10 [o]Mnamo majira
ya vuli, Mfalme Nebukadneza akatuma
watu, nao wakamleta Babeli, pamoja na
vyombo vya thamani kutoka Hekalu la
Bwana. Naye akamfanya Sedekia, ndugu
yake Yehoyakimu kuwa mfalme wa Yuda
na Yerusalemu.

[a]**35:23** 1Fal 22:34; Dan 2:21
[b]**35:24** 2Fal 23:30; Zek 12:11
[c]**35:25** Mwa 50:10; Yer 22:10-16; Mao 4:20; Mt 9:23; Amo 5:16; Mhu 12:5; Yer 9:17
[d]**35:26** Za 112:6; Mit 10:7; 22:1
[e]**36:1** 2Fal 23:30; 2Nya 33:25
[f]3 Talanta 100 za fedha ni sawa na tani 3.75.
[g]3 Talanta moja ya dhahabu ni sawa na kilo 34.
[h]**36:4** Yer 22:10-12; Eze 19:3
[i]**36:5** Yer 25:1; 36:1, 27-32; 2Fal 23:36-37
[j]**36:6** Yer 25:9; Eze 29:18; 19:9; 2Fal 24:1-6; Hab 1:6-10
[k]**36:7** 2Fal 24:13; Yer 27:16
[l]7 Au: katika jumba lake la kifalme.
[m]**36:8** 1Nya 3:16
[n]**36:9** 2Fal 24:8; Yer 24:1; 27:16
[o]**36:10** Isa 52:11; Dan 5:2

*Mfalme Sedekia Wa Yuda*

**(2 Wafalme 24:18-20; Yeremia 52:1-3)**

11 [a]Sedekia alikuwa na umri wa miaka ishirini na mmoja alipoanza kutawala, naye akatawala huko Yerusalemu kwa miaka kumi na mmoja. 12 [b]Alifanya maovu machoni pa Bwana Mungu wake, wala hakujinyenyekeza mbele ya nabii Yeremia, ambaye alinena neno la Bwana. 13 [c]Pia alimwasi Mfalme Nebukadneza, ambaye alikuwa amemwapisha kwa jina la Mungu. Akashupaza shingo na akafanya moyo wake kuwa mgumu wala hakutaka kumgeukia Bwana, Mungu wa Israeli. 14 [d]Zaidi ya hayo viongozi wote wa makuhani pamoja na watu wakazidi kukosa uaminifu zaidi na zaidi, wakafanya machukizo yote kama walivyofanya mataifa wakinajisi Hekalu la Bwana alilokuwa amelitakasa huko Yerusalemu.

*Kuanguka Kwa Yerusalemu*

**(2 Wafalme 25:1-21; Yeremia 52:3-11)**

15 [e]Bwana, Mungu wa baba zao, akawapelekea neno kupitia wajumbe wake tena na tena, kwa sababu alikuwa anawahurumia watu wake pamoja na mahali pa maskani yake. 16 [f]Lakini waliwadhihaki wajumbe wa Bwana wakayadharau maneno yake na kuwacheka manabii wake mpaka ghadhabu ya Bwana ikawa kubwa dhidi ya watu wake na hakukuwa na namna ya kuituliza. 17 [g]Mungu akamwinua dhidi yao mfalme wa Wakaldayo, aliyewaua vijana wao wa kiume kwa upanga ndani ya mahali patakatifu, ambaye hakumbakiza kijana mwanaume wala kijana mwanamke, wazee wala vikongwe. Mungu akawatia wote mikononi mwa Nebukadneza. 18 [h]Akavichukua kwenda Babeli vyombo vyote kutoka Hekalu la Mungu, vikubwa na vidogo, hazina za Hekalu la Bwana pamoja na hazina za mfalme na za maafisa wake. 19 [i]Wakalichoma Hekalu la Mungu na kuzibomoa kuta za Yerusalemu, wakachoma moto majumba yote ya kifalme na kuharibu kila kitu chake cha thamani.

20 [j]Wale watu walionusurika kuuawa kwa upanga wakachukuliwa kwenda uhamishoni Babeli. Nao wakawa watumishi wake na wa wanawe mpaka wakati wa utawala wa ufalme wa Uajemi ulifika. 21 [k]Nchi ikaendelea kufurahia pumziko lake la Sabato, wakati wote wa kufanywa kwake ukiwa ilipumzika mpaka ile miaka sabini ilipotimia katika kutimiza neno la Bwana lililonenwa na Yeremia.

*Koreshi Atangaza Uhuru Kwa Waliokuwa Uhamishoni*

**(Ezra 1:1-4)**

22 [l]Katika mwaka wa kwanza wa utawala wa Koreshi mfalme wa Uajemi, ili kulitimiza neno la Bwana lililosemwa na nabii Yeremia, Bwana aliusukuma moyo wa Koreshi mfalme wa Uajemi kutangaza katika himaya yake yote kwa maandishi:

> 23 "Hili ndilo asemalo Koreshi mfalme wa Uajemi:
>
> " 'Bwana, Mungu wa mbinguni, amenipa falme zote duniani, na ameniagiza kumjengea Hekalu huko Yerusalemu katika Yuda. Yeyote wa watu wake miongoni mwenu, Mungu wake na awe pamoja naye, wacha huyo mtu na apande.' "

---

[a]**36:11** 2Fal 24:17; Yer 39:1
[b]**36:12** Yer 39:18; Kum 8:3; Yer 21:3-7
[c]**36:13** Eze 17:13; Kut 32:9; 2Fal 17:14; Neh 8:16-17; Yer 52:3; Kut 17:15
[d]**36:14** 1Nya 5:25
[e]**36:15** Hag 1:13; Yer 11:7; 44:4-6; Hos 11:8; Yer 25:3
[f]**36:16** Mit 1:25-31; Mik 2:11; Yer 7:26; Dan 9:6; Lk 16:14
[g]**36:17** Yer 9:21; 18:21; Mao 2:21; Eze 9:6
[h]**36:18** Yer 17:20; 2Fal 25:13
[i]**36:19** Amo 2:5; 1Fal 9:8-9; 14:13; Mao 2:6; Za 79:1-3
[j]**36:20** Ezr 2:1; Neh 7:6; Yer 27:7
[k]**36:21** Law 25:4; 26:34
[l]**36:22** Yer 29:10; Isa 44:28

# EZRA

*Koreshi Asaidia Watu Kurudi Kutoka Uhamishoni*

1 [a]Katika mwaka wa kwanza wa utawala
wa Koreshi mfalme wa Uajemi, ili
kulitimiza neno la Bwana lililosemwa na
nabii Yeremia, Bwana aliusukuma moyo
wa Koreshi mfalme wa Uajemi kutangaza
katika himaya yake yote kwa maandishi:

> 2 [b]"Hili ndilo asemalo Koreshi mfalme
> wa Uajemi:
>
> " 'Bwana, Mungu wa mbinguni,
> amenipa falme zote duniani, na
> ameniagiza kumjengea Hekalu huko
> Yerusalemu katika Yuda. 3 [c]Yeyote wa
> watu wake miongoni mwenu, Mungu
> wake na awe pamoja naye, wacha
> apande kwenda Yerusalemu katika
> Yuda na kujenga Hekalu la Bwana,
> Mungu wa Israeli, Mungu aliyeko huko
> Yerusalemu. 4 [d]Nao watu wa mahali
> popote wale walionusurika wanapoishi
> sasa, watu hao wampe fedha na
> dhahabu, pamoja na vifaa na mifugo,
> mbali na sadaka za hiari kwa ajili ya
> Hekalu la Mungu huko Yerusalemu.' "

5 [e]Kisha viongozi wa jamaa ya Yuda na
Benyamini na makuhani na Walawi kila
mmoja ambaye moyo wake ulisukumwa
na Mungu, akajiandaa kupanda ili kuijenga
nyumba ya Bwana huko Yerusalemu.
6 Majirani zao wote wakawasaidia
vyombo vya fedha na dhahabu, pamoja
na vifaa na mifugo, pia na zawadi za
thamani, pamoja na sadaka zote za hiari.
7 [f]Zaidi ya hayo, Mfalme Koreshi akavitoa
vyombo vilivyokuwa mali ya Hekalu la
Bwana, ambavyo Nebukadneza alikuwa
amevichukua kutoka Yerusalemu na
kuviweka katika hekalu la mungu wake.
8 [g]Koreshi mfalme wa Uajemi akavitoa kwa
mkono wa Mithredathi mtunza hazina,
aliyevihesabu mbele ya Sheshbaza mkuu
wa Yuda.

9 Hii ilikuwa ndio orodha ya vifaa:

| | |
|---|---|
| masinia ya dhahabu yalikuwa | 30 |
| masinia ya fedha yalikuwa | 1,000 |
| vyetezo vya fedha vilikuwa | 29 |
| 10 mabakuli ya dhahabu yalikuwa | 30 |
| mabakuli ya fedha yanayofanana yalikuwa | 410 |
| vifaa vingine vilikuwa | 1,000. |

11 Kwa ujumla, kulikuwa na vyombo
5,400 vya dhahabu na vya fedha. Sheshbaza
akavileta hivi vyote wakati watu walipotoka
uhamishoni Babeli kwenda Yerusalemu.

*Orodha Ya Watu Waliorudi Kutoka Uhamishoni*

**(Nehemia 7:4-73)**

2 [h]Basi hawa ndio watu wa jimbo
waliotoka uhamishoni, ambao
Nebukadneza mfalme wa Babeli
alikuwa amewachukua mateka
hadi Babeli (walirudi Yerusalemu
na Yuda, kila mmoja kwenye mji
wake, 2 [i]wakiwa wamefuatana
na Zerubabeli, Yeshua, Nehemia,
Seraya, Reelaya, Mordekai, Bilshani,
Mispari, Bigwai, Rehumu na Baana):

Orodha ya wanaume kati ya watu
wa Israeli ilikuwa:

---

[a]**1:1** Yer 29:10-14; Zek 1:12-16; 2Nya 36:22-23; Ezr 5:13; 7:27; Yer 25:12; Law 26:42
[b]**1:2** Amu 4:10; Isa 44:28; Ezr 5:13; Za 72:11
[c]**1:3** Kum 3:24; 2Sam 22:32; Za 86:10; Dan 6:26; 1Kor 8:6; Isa 37:16; Mk 12:32
[d]**1:4** Isa 10:20-22; Hes 15:3; Za 116:17; Ezr 3:7; 4:3
[e]**1:5** 2Nya 34:9; Neh 12:34; Hag 1:4; Flp 2:13; Mit 16:1
[f]**1:7** 2Fal 24:13; Ezr 5:14; 6:5; 2Nya 36:7; Yer 52:17-19
[g]**1:8** Ezr 5:14; Hag 1:1; 1Nya 3:18
[h]**2:1** 2Nya 36:20; Neh 7:6; 11:3; 2Fal 24:16; 25:12; Ezr 5:8; 6:2; Es 1:1; 8:9
[i]**2:2** 1Nya 3:19; 6:14; Hag 2:4; Zek 3:1-10

3 [a]wazao wa Paroshi 2,172
4 wazao wa Shefatia 372
5 [b]wazao wa Ara 775
6 wazao wa Pahath-Moabu (wa jamaa ya Yeshua na Yoabu) 2,812
7 wazao wa Elamu 1,254
8 wazao wa Zatu 945
9 wazao wa Zakai 760
10 wazao wa Bani 642
11 wazao wa Bebai 623
12 wazao wa Azgadi 1,222
13 [c]wazao wa Adonikamu 666
14 wazao wa Bigwai 2,056
15 wazao wa Adini 454
16 wazao wa Ateri (kupitia Hezekia) 98

17 wazao wa Besai 323
18 wazao wa Yora 112
19 wazao wa Hashumu 223
20 [d]wazao wa Gibari 95

21 [e]watu wa Bethlehemu 123
22 watu wa Netofa 56
23 watu wa Anathothi 128
24 watu wa Azmawethi 42
25 wazao wa Kiriath-Yearimu, Kefira na Beerothi 743
26 [f]wazao wa Rama na Geba 621
27 watu wa Mikmashi 122
28 [g]watu wa Betheli na Ai 223
29 wazao wa Nebo 52
30 wazao wa Magbishi 156
31 [h]wazao wa Elamu ile ingine 1,254
32 wazao wa Harimu 320
33 wazao wa Lodi, Hadidi na Ono 725
34 [i]wazao wa Yeriko 345
35 wazao wa Senaa 3,630

36 [j]Makuhani:
wazao wa Yedaya (kwa jamaa ya Yeshua) 973
37 [k]wazao wa Imeri 1,052
38 [l]wazao wa Pashuri 1,247
39 [m]wazao wa Harimu 1,017

40 [n]Walawi:
wazao wa Yeshua na Kadmieli (kupitia jamaa ya Hodavia) 74

41 [o]Waimbaji:
wazao wa Asafu 128

42 [p]Mabawabu wa lango la Hekalu:
wazao wa Shalumu, Ateri, Talmoni, Akubu, Hatita na Shobai 139

43 [q]Watumishi wa Hekalu:[r]
wazao wa Siha, Hasufa, Tabaothi,
44 wazao wa Kerosi, Siaha, Padoni,
45 wazao wa Lebana, Hagaba, Akubu,
46 wazao wa Hagabu, Shalmai, Hanani,
47 wazao wa Gideli, Gahari, Reaya,
48 wazao wa Resini, Nekoda, Gazamu,
49 wazao wa Uza, Pasea, Besai,
50 wazao wa Asna, Meunimu, Nefusimu,
51 wazao wa Bakbuki, Hakufa, Harhuri,
52 wazao wa Basluthi, Mehida, Harsha,
53 wazao wa Barkosi, Sisera, Tema,
54 wazao wa Nesia na Hatifa.

55 [s]Wazao wa watumishi wa Solomoni:
wazao wa Sotai, Hasaferethi, Peruda,
56 wazao wa Yaala, Darkoni, Gideli,
57 wazao wa Shefatia, Hatili, Pokereth-Hasebaimu na Ami.

58 [t]Watumishi wa Hekalu wote na wazao wa watumishi wa Solomoni 392

59 [u]Wafuatao walikuja kutoka miji ya Tel-Mela, Tel-Harsha, Kerubu,

[a]**2:3** Ezr 10:25; Neh 3:25
[b]**2:5** Neh 6:18
[c]**2:13** Ezr 8:13; 7:18
[d]**2:20** Yos 9:17
[e]**2:21** Mik 5:2; 1Nya 2:51; Rut 1:19; Mt 2:6; 2Sam 21:2; Mwa 35:19
[f]**2:26** Yos 18:25; 1Sam 7:17; Yer 31:15
[g]**2:28** Mwa 12:8
[h]**2:31** Ezr 2:7
[i]**2:34** Kum 34:3; 2Nya 28:15; 1Fal 16:34
[j]**2:36** 1Nya 9:10; 24:7
[k]**2:37** 1Nya 24:14; Ezr 10:20
[l]**2:38** 1Nya 9:12; Ezr 10:22
[m]**2:39** 1Nya 24:8
[n]**2:40** Mwa 29:34; Hes 3:9; Ezr 3:9
[o]**2:41** 1Nya 15:16
[p]**2:42** 1Sam 3:15; 1Nya 9:17
[q]**2:43** 1Nya 9:2
[r]43 Yaani *Wanethini* (pia 2:58, 70).
[s]**2:55** 1Fal 9:21
[t]**2:58** 1Fal 9:21; Ezr 7:7; Yos 9:21-27; 1Nya 9:2
[u]**2:59** Hes 1:18

Adoni na Imeri, lakini hawakuweza kuthibitisha kwamba jamaa zao zilikuwa uzao wa Israeli:
60 wazao wa Delaya, Tobia na Nekoda 652

61 [a]Kutoka miongoni mwa makuhani: Wazao wa Hobaya, Hakosi, Barzilai (mtu aliyekuwa amemwoa binti wa Barzilai, Mgileadi, naye akaitwa kwa jina hilo).
62 [b]Hawa walitafuta orodha za jamaa zao, lakini hawakuonekana humo, kwa hiyo waliondolewa kutoka kundi la makuhani kwa kuwa walihesabiwa kuwa najisi.
63 [c]Mtawala aliagiza kuwa wasile chochote miongoni mwa vyakula vitakatifu hadi kuwe kuhani atakayehudumu kwa Urimu na Thumimu.[d]

64 Jumla ya watu wote waliorudi walikuwa 42,360;
65 [e]tena zaidi ya hao walikuwepo watumishi wa kiume na wa kike 7,337; pia walikuwamo waimbaji wanaume na wanawake 200.
66 [f]Walikuwa na farasi 736, nyumbu 245,
67 ngamia 435 na punda 6,720.

68 [g]Walipofika kwenye nyumba ya BWANA
huko Yerusalemu, baadhi ya viongozi wa
jamaa walitoa sadaka za hiari kwa ajili ya
kujenga upya nyumba ya Mungu katika
eneo lake.
69 Wakatoa kwa kadiri ya uwezo
wao na kutia katika hazina darkoni 61,000[h]
za dhahabu, mane 5,000[i] za fedha, na
mavazi 100 ya ukuhani kwa ajili ya kazi
hiyo.
70 [j]Makuhani, Walawi, waimbaji,
mabawabu, na watumishi wa Hekalu
waliishi katika miji yao wenyewe, pamoja
na baadhi ya watu wengine, nao Waisraeli
waliosalia waliishi katika miji yao.

*Madhabahu Yajengwa Tena*

3 [k]Mwezi wa saba ulipowadia baada ya
Waisraeli kukaa katika miji yao, watu
wote walikusanyika huko Yerusalemu
kama mtu mmoja.
2 [l]Yeshua mwana wa
Yosadaki na makuhani wenzake, Zerubabeli
mwana wa Shealtieli pamoja na wenzake
walianza kujenga madhabahu ya Mungu wa
Israeli ili kumtolea dhabihu za sadaka za
kuteketezwa kwa moto juu yake, kulingana
na ilivyoandikwa katika Sheria ya Mose mtu
wa Mungu.
3 [m]Ingawa waliwaogopa watu
waliowazunguka, walijenga madhabahu juu
ya ule msingi wake, wakamtolea BWANA
dhabihu za sadaka za kuteketezwa kwa
moto juu yake za asubuhi na za jioni.
4 [n]Kisha kulingana na kile kilichoandikwa,
wakaiadhimisha Sikukuu ya Vibanda
wakitoa idadi ya sadaka za kuteketezwa
kama ilivyohitajika kila siku sawasawa na
ilivyoagizwa.
5 [o]Baada ya hayo, walitoa
sadaka za kuteketezwa za kawaida, sadaka
za Mwezi Mwandamo na dhabihu zote za
sikukuu takatifu za BWANA zilizoamriwa,
pamoja na zile sadaka za hiari zilizotolewa
kwa BWANA.
6 Ingawa bado msingi wa
Hekalu la BWANA ulikuwa haujawekwa,
watu walianza kutoa sadaka za kuteketezwa

[a]**2:61** 2Sam 17:27; 1Fal 2:7
[b]**2:62** Hes 16:39-40; 3:10
[c]**2:63** Neh 8:9; Hes 18:9-11; Kut 28:30; Law 2:3-10
[d]63 Urimu na Thumimu maana yake ni Nuru na Kweli; vifaa hivi viliwekwa kwenye kifuko cha kifuani cha kisibau cha kuhani mkuu ili kujua mapenzi ya Mungu kwenye mambo ya kutatanisha.
[e]**2:65** 2Sam 19:35
[f]**2:66** Isa 66:20
[g]**2:68** Kut 15:2
[h]69 Darkoni 61,000 za dhahabu ni sawa na kilo 500.
[i]69 Mane 5,000 za fedha ni sawa na kilo 2,900.
[j]**2:70** 1Nya 9:2; Neh 11:3-4
[k]**3:1** Neh 7:73; Law 23:24
[l]**3:2** Zek 3:1; Ezr 2:2; Mt 1:12; Lk 3:27; Zek 6:11; Hag 2:2; Kut 20:24; Kum 12:5-6; Neh 12:1-8
[m]**3:3** Kut 29:38-42; Hes 28:1-8; Dan 9:25; Ezr 4:4
[n]**3:4** Kut 23:16; Zek 14:16; Hes 29:12-38; Neh 8:14
[o]**3:5** Hes 28:3-11; Kol 2:16; Kut 29:38; Law 23:1-44; Hes 29:39

kwa moto kwa BWANA tangu siku ya
kwanza ya mwezi wa saba.

*Kujenga Upya Hekalu*

7 [a]Kisha watu wakawapa mafundi wa
uashi na useremala fedha, wakawapa
watu wa Sidoni na Tiro vyakula, vinywaji
na mafuta ili waweze kuleta magogo ya
mierezi kwa njia ya bahari kutoka Lebanoni
hadi Yafa, kama alivyoagiza Koreshi mfalme
wa Uajemi.
8 [b]Katika mwezi wa pili wa mwaka wa pili
baada ya Waisraeli kufika kwenye nyumba
ya Mungu huko Yerusalemu, Zerubabeli
mwana wa Shealtieli, Yeshua mwana wa
Yosadaki na ndugu zao wengine (makuhani,
Walawi na wote waliorejea Yerusalemu
kutoka uhamishoni) walianza kazi, wakiteua
Walawi wenye umri kuanzia miaka ishirini
au zaidi kusimamia ujenzi wa nyumba ya
BWANA. 9 [c]Yeshua na wanawe, pamoja na
ndugu zake, Kadmieli na wanawe (wazao
wa Hodavia), wana wa Henadadi na wana
wao na ndugu zao, Walawi wote walijiunga
pamoja kusimamia wale waliofanya kazi
katika nyumba ya Mungu.
10 [de]Wajenzi walipoweka msingi wa
Hekalu la BWANA, makuhani wakiwa
wamevalia mavazi yao wakiwa na
tarumbeta na Walawi (wana wa Asafu)
wakiwa na matoazi, walishika nafasi zao
za kumtukuza BWANA, kama ilivyoagizwa
na Daudi mfalme wa Israeli. 11 [f]Waliimba
nyimbo za sifa na za shukrani kwa BWANA
hivi:

"Yeye ni mwema;
upendo wake kwa Israeli
wadumu milele."

Watu wote wakapaza sauti kubwa za
sifa kwa BWANA, kwa sababu msingi wa
nyumba ya BWANA ulikuwa umewekwa.
12 [g]Lakini wengi wa makuhani wazee,
Walawi na viongozi wa jamaa waliokuwa
wameona Hekalu la mwanzoni, walilia
kwa sauti walipoona msingi wa Hekalu hili
ukiwekwa, huku wengine wengi wakipiga
kelele kwa furaha. 13 [h]Hakuna mtu ambaye
angeweza kutofautisha sauti hizo za furaha
na za kilio, kwa sababu watu walipiga
kelele sana. Nayo hiyo sauti ikasikika mbali.

*Upinzani Kuhusu Ujenzi Mpya*

4 Adui za Yuda na Benyamini waliposikia
kwamba watu waliorudi kutoka
uhamishoni wanajenga Hekalu kwa ajili
ya BWANA, Mungu wa Israeli, 2 [i]wakamjia
Zerubabeli na viongozi wa jamaa, nao
wakasema, "Turuhusuni tuwasaidie
kujenga, kwa sababu sisi tunamtafuta
Mungu wenu kama ninyi na tumekuwa
tukimtolea dhabihu tangu wakati wa Esar-
Hadoni mfalme wa Ashuru, aliyetuleta
hapa."
3 [j]Lakini Zerubabeli, Yeshua na viongozi
wengine wa jamaa ya Israeli wakawajibu,
"Ninyi hamna sehemu nasi katika kujenga
Hekalu la Mungu wetu. Sisi peke yetu
tutajenga Hekalu kwa ajili ya BWANA,
Mungu wa Israeli, kama Mfalme Koreshi,
mfalme wa Uajemi alivyotuagiza."
4 [k]Ndipo watu waliowazunguka
wakajipanga kuwakatisha tamaa watu wa
Yuda na kuwafanya waogope walipokuwa
wakiendelea na ujenzi. 5 Wakaajiri washauri
kuwapinga katika kazi yao, nao wakaipinga
mipango yao wakati wote wa utawala wa
Koreshi mfalme wa Uajemi hadi wakati wa
utawala wa Dario mfalme wa Uajemi.

*Upinzani Mwingine Chini Ya Ahasuero Na Artashasta*

6 [l]Mnamo mwanzo wa utawala wa

---

[a]**3:7** 1Nya 14:1; Isa 35:2; Ezr 6:3; 2Nya 2:10; Mdo 9:36; 12:20; Isa 60:13
[b]**3:8** Zek 4:9; Hes 4:3; 1Nya 23:24-27
[c]**3:9** Ezr 2:40
[d]**3:10** Zek 6:12; Ezr 6:3; 1Nya 15:27-28; 6:31; Hag 2:15
[e]**3:10** 2Nya 5:13; 1Nya 6:31
[f]**3:11** 1Nya 16:34; Za 138:8; Yos 6:5-10; Neh 12:24; 2Nya 7:3; Yer 33:11; Lk 1:50; Za 136:1; Kut 15:21
[g]**3:12** Hag 2:3-9
[h]**3:13** Ay 33:26; Yer 48:33
[i]**4:2** Es 8:17; 2Fal 17:24, 41; 19:37
[j]**4:3** Yn 4:9; 2Nya 36:22-23; Ezr 1:1-4; 6:3; Isa 44:28; Neh 2:20; Mdo 8:21
[k]**4:4** Ezr 3:3; Yer 38:4; Isa 35:3-4
[l]**4:6** Es 3:13; 9:5; Dan 9:1

Ahasuero, hao adui waliandika mashtaka
dhidi ya watu wa Yuda na Yerusalemu.
7 [a]Pia katika siku za utawala wa
Artashasta mfalme wa Uajemi, Bishlamu,
Mithredathi, Tabeeli pamoja na wenzao
waliandika barua kwa Artashasta. Barua
hiyo iliandikwa kwa mwandiko wa Kiaramu
na katika lugha ya Kiaramu.
8 [b]Rehumu afisa msimamizi na mwandishi
Shimshai waliandika barua kwa Mfalme
Artashasta dhidi ya watu wa Yerusalemu
kama ifuatavyo:

9 [c]Rehumu afisa msimamizi na
mwandishi Shimshai, pamoja na
wenzao, yaani mahakimu na maafisa
walio juu ya watu kuanzia Tripoli,
Uajemi, Ereki na Babeli, Waelami
wa Shushani, 10 [d]na watu wengine
ambao mheshimiwa Asur-Banipali[e]
aliwahamisha na kuwakalisha katika
mji wa Samaria na mahali pengine
Ng'ambo ya Mto Frati.

11 (Hii ndiyo nakala ya barua
waliyompelekea.)

Kwa Mfalme Artashasta,

Kutoka kwa watumishi wako, watu wa
Ng'ambo ya Mto Frati:

12 [f]Yapasa Mfalme ajue kuwa
Wayahudi waliopanda kuja kwetu
kutoka kwenu, wamekwenda
Yerusalemu nao wanaujenga upya ule
mji wa uasi na uovu. Wanajenga kuta
upya na kukarabati misingi yake.
13 [g]Zaidi ya hayo, mfalme yampasa
ajue kwamba kama mji huu ukijengwa
na kuta zake zikafanywa upya,
hakutakuwa na ulipaji wa kodi wala
ada au ushuru, hivyo hazina za mfalme
zitaathirika. 14 Sisi sasa kwa kuwa
tunawajibika kwa jumba la kifalme na
kwamba siyo sawasawa kwetu kuona
mfalme akidharauliwa, basi tunatuma
ujumbe huu kumtaarifu mfalme, 15 [h]ili
kwamba ufanyike uchunguzi kwenye
kumbukumbu ya maandishi ya
waliokutangulia. Katika kumbukumbu
hizi utagundua kwamba mji huu ni
wa maasi, unaowataabisha wafalme
na majimbo, ni mahali pa maasi
tangu zamani. Ndiyo maana mji huu
uliharibiwa. 16 Tunamjulisha mfalme
kwamba kama mji huu ukijengwa na
kuta zake zikifanywa upya, hutabakiwa
na chochote Ng'ambo ya Mto Frati.

17 Mfalme alirudisha jibu hili:

Kwa Rehumu, afisa msimamizi,
mwandishi Shimshai na wenzenu
wote wanaoishi katika Samaria na
penginepo Ng'ambo ya Mto Frati:

Salamu.

18 Barua mliyotutumia imesomwa
na kutafsiriwa mbele yangu. 19 [i]Nilitoa
amri na uchunguzi ukafanyika na
imegundulika kwamba mji huu una
historia ndefu ya maasi dhidi ya
wafalme na pamekuwa mahali pa
maasi na uchochezi. 20 [j]Yerusalemu
umepata kuwa na wafalme wenye
nguvu wakitawala nchi yote iliyo
Ng'ambo ya Mto Frati, wakitoza kodi,
ada na ushuru huko. 21 Kwa hiyo toeni
amri kwa watu hawa wasimamishe
ujenzi, ili kwamba mji huu usiendelee
kujengwa hadi nitakapoagiza. 22 [k]Mwe
waangalifu msipuuze jambo hili. Kwa
nini kuruhusu tishio hili kuendelea na
kusababisha hasara kwa ufalme?

23 [l]Mara waliposomewa nakala ya
barua ya Mfalme Artashasta, Rehumu na
Shimshai aliyekuwa mwandishi na wenzao,
walikwenda mara moja kwa Wayahudi
huko Yerusalemu na kuwalazimisha kwa
nguvu kusimamisha ujenzi.

---

[a]**4:7** Ezr 7:1; Isa 36:11; Neh 2:1
[b]**4:8** Za 112:6; Zek 1:14; Rum 8:28
[c]**4:9** Ezr 5:6; 2Fal 17:30, 31
[d]**4:10** Neh 4:2; Ezr 7:12
[e]10 Yaani Osnapali au Asnapali kwa Kiaramu.
[f]**4:12** Amo 7:10; Lk 23:2; Mdo 24:5
[g]**4:13** Ezr 7:24; Neh 5:4; Mt 9:9
[h]**4:15** Ezr 5:17; Es 3:8; Mdo 17:6-7
[i]**4:19** 2Fal 18:7
[j]**4:20** Mwa 15:18-21; Kut 23:31; Za 72:8; 1Nya 18:3
[k]**4:22** Dan 6:2
[l]**4:23** Mit 4:16

24 [a]Hivyo kazi ya ujenzi wa nyumba ya
Mungu huko Yerusalemu ikasimamishwa
kabisa hadi mwaka wa pili wa utawala wa
Dario mfalme wa Uajemi.

*Barua Ya Tatenai Kwa Dario*

5 [b]Ndipo nabii Hagai na nabii Zekaria
mzao wa Ido, wakawatolea unabii
Wayahudi waliokuwa Yuda na Yerusalemu
kwa jina la Mungu wa Israeli, aliyekuwa
pamoja nao. 2 [c]Ndipo Zerubabeli mwana wa
Shealtieli na Yeshua mwana wa Yosadaki
wakaanza kujenga tena nyumba ya Mungu
huko Yerusalemu. Nao manabii wa Mungu
walikuwa pamoja nao, wakiwasaidia.
3 [d]Wakati ule Tatenai mtawala wa
ng'ambo ya mto Frati na Shethar-Bozenai
na wenzao waliwaendea, wakawauliza,
"Ni nani aliyewapa ruhusa ya kujenga
tena Hekalu hili na kurudishia upya kama
lilivyokuwa?" 4 Pia waliwauliza, "Je,
majina ya watu wanaofanya ujenzi huu
ni nani?" 5 [e]Lakini jicho la Mungu wao
lilikuwa likiwaangalia wazee wa Wayahudi,
nao hawakuzuiliwa kujenga mpaka taarifa
ikaandikwa kwa Dario na majibu yake
kupokelewa.
6 [f]Hii ni nakala ya barua ile Tatenai,
mtawala wa ng'ambo ya mto Frati na
Shethar-Bozenai na wenzao maafisa wa
ng'ambo ya mto Frati waliyompelekea
Mfalme Dario. 7 Taarifa waliyompelekea
ilisomeka kama ifuatavyo:

Kwa Mfalme Dario:

Salamu kwa moyo mkunjufu.

8 Inampasa Mfalme ajue kwamba
tulikwenda katika eneo la Yuda,
kwenye Hekalu la Mungu mkuu. Watu
wanalijenga kwa mawe makubwa
na kuweka mbao kwenye kuta. Kazi
inafanyika kwa bidii na inaendelea
kwa haraka chini ya uongozi wao.
9 [g]Tuliwauliza viongozi, "Ni nani
aliyewapa ruhusa kujenga upya Hekalu
hili na kurejeza hali ya jengo kama
lilivyokuwa?" 10 Pia tuliwauliza majina
yao, ili tukuandikie kukujulisha majina
ya viongozi wao.
11 [h]Hili ndilo jibu walilotupa:

"Sisi ni watumishi wa Mungu wa
mbingu na nchi, nasi tunalijenga
upya Hekalu ambalo lilijengwa
miaka mingi iliyopita, lile ambalo
mfalme mkuu wa Israeli alilijenga na
kulikamilisha. 12 [i]Lakini kwa sababu
baba zetu walimkasirisha Mungu wa
mbinguni, basi aliwatia mkononi mwa
Nebukadneza, Mkaldayo, mfalme wa
Babeli, ambaye aliliharibu Hekalu hili
na kuwaondoa watu na kuwapeleka
uhamishoni huko Babeli.
13 [j]"Pamoja na hayo, katika mwaka
wa kwanza wa kutawala Koreshi
mfalme wa Babeli, Mfalme Koreshi
alitoa amri ya kujengwa upya nyumba
hii ya Mungu. 14 [k]Yeye hata aliviondoa
vyombo vya dhahabu na fedha vya
nyumba ya Mungu, kutoka Hekalu la
Babeli ambavyo Nebukadneza alikuwa
amevichukua kutoka ndani ya Hekalu
huko Yerusalemu na kuvileta katika
Hekalu la Babeli.
"Vyombo hivyo Mfalme Koreshi
alimkabidhi mtu aliyeitwa Sheshbaza,
ambaye Koreshi alikuwa amemteua
awe mtawala, 15 naye akamwambia,
'Chukua vyombo hivi uende ukaviweke
ndani ya Hekalu huko Yerusalemu.
Nawe uijenge upya nyumba ya Mungu
mahali pake.' 16 [l]Hivyo huyu Sheshbaza
alikuja na kuweka misingi ya nyumba
ya Mungu iliyoko Yerusalemu. Tangu

[a]**4:24** Dan 9:25; Ay 20:5
[b]**5:1** Ezr 6:14; Hag 1:14; Zek 8:9
[c]**5:2** 1Nya 3:19; Ezr 6:14; Mhu 12:11; Zek 4:6-10; Hag 1:2-15; 2:2-5
[d]**5:3** Ezr 6:6
[e]**5:5** 2Fal 25:28; 1Pet 3:12; 2Nya 16:9; Ezr 7:6, 28; Za 33:18; Isa 41:10
[f]**5:6** Ezr 4:9
[g]**5:9** Ezr 4:12
[h]**5:11** 1Fal 6:1; Yos 24:15; Za 119:46; Yn 1:9; Mt 10:32; Lk 12:8; Mdo 27:23; 2Nya 3:1, 2
[i]**5:12** 2Nya 34:24-25; 36:16, 17; Yer 39:1; 2Fal 24:2
[j]**5:13** Ezr 1:1
[k]**5:14** Ezr 6:5; Dan 5:2; 1Nya 3:18; Hag 1:4
[l]**5:16** Ezr 3:10; 6:15; 4:15; 6:1-2

siku hiyo hadi sasa imekuwa ikiendelea kujengwa lakini bado haijamalizika."

17 [a]Sasa kama ikimpendeza mfalme, uchunguzi na ufanyike katika kumbukumbu za maandishi ya ufalme mjini Babeli, kuona kama kweli Mfalme Koreshi alitoa amri ya kujenga upya nyumba ya Mungu katika Yerusalemu. Kisha tunaomba mfalme na atutumie uamuzi wake kuhusu jambo hili.

*Amri Ya Dario*

6 [b]Kisha Mfalme Dario alitoa amri, nao wakafanya uchunguzi katika kumbukumbu zilizohifadhiwa katika hazina huko Babeli.
2 Karatasi moja ndefu ya maandishi ilipatikana huko Ekbatana katika jimbo la Umedi. Haya ndiyo yaliyokuwa yameandikwa humo:

Kumbukumbu:

3 [c]Katika mwaka wa kwanza wa kutawala Mfalme Koreshi, mfalme alitoa amri kuhusu Hekalu la Mungu katika Yerusalemu:

Hekalu na lijengwe tena mahali palepale Wayahudi walipokuwa wakitoa dhabihu, kwenye msingi ule ule. Iwe na kimo cha mikono sitini,[d]
upana wa mikono sitini,
4 [e]kuta zijengwe kwa safu tatu za mawe makubwa kisha ifuate safu moja ya mbao. Gharama zitalipwa kutoka hazina ya mfalme.
5 [f]Pia, vyombo vya dhahabu na vya fedha vya nyumba ya Mungu, ambavyo Nebukadneza alivichukua kutoka kwenye Hekalu huko Yerusalemu akavileta Babeli, yapasa virudishwe mahali pake ndani ya Hekalu huko Yerusalemu, yapasa viwekwe ndani ya nyumba ya Mungu.

6 [g]Sasa basi, Tatenai, mtawala wa Ng'ambo ya Mto Frati na Shethar-Bozenai pamoja na ninyi, maafisa wenzao wa jimbo hilo kaeni mbali na mahali hapo.
7 Msiingilie kazi ya Hekalu hili la Mungu. Mwacheni mtawala wa Wayahudi na viongozi Wayahudi wajenge upya nyumba hii ya Mungu mahali pake.
8 [h]Zaidi ya hayo, hapa natoa amri kuhusu mtakalofanya kwa ajili ya wazee wa Wayahudi katika ujenzi wa nyumba hii ya Mungu:

Gharama za watu hawa zitalipwa kikamilifu kutoka hazina ya mfalme, kutoka kwenye mapato ya Ng'ambo ya Mto Frati, ili ujenzi usisimame.
9 Chochote kinachohitajika kama mafahali wachanga, kondoo dume, wana-kondoo kwa ajili ya sadaka za kuteketezwa kwa Mungu wa mbinguni, ngano, chumvi, divai na mafuta kama vitakavyohitajika na makuhani huko Yerusalemu, lazima wapewe kila siku pasipo kukosa,
10 [i]ili waweze kutoa dhabihu inayompendeza Mungu wa mbinguni na kumwombea mfalme na wanawe hali njema.
11 [j]Zaidi ya hayo, ninaamuru kwamba mtu yeyote atakayebadilisha amri hii, boriti itang'olewa kutoka nyumba yake, ichongwe upande mmoja na atumbuliwe nayo. Kwa ajili ya kosa hili nyumba yake ifanywe lundo la taka.
12 [k]Naye Mungu, aliyeliweka Jina lake huko, amwangushe mfalme yeyote au watu watakaoinua mikono kubadili amri hii au kuharibu Hekalu hili lililoko Yerusalemu.

Mimi Dario nimetoa amri hii. Nayo itekelezwe kwa bidii na kwa makini.

[a]**5:17** Ezr 6:1, 2; Mit 25:2
[b]**6:1** Ezr 4:15; 5:17
[c]**6:3** Ezr 3:10; Hag 2:3
[d]3 Mikono 60 ni sawa na mita 27.
[e]**6:4** 1Fal 6:36; Ezr 7:20; Isa 60:6; Za 68:29
[f]**6:5** 1Nya 29:2; Yer 27:18-22; Ezr 5:14
[g]**6:6** Ezr 5:3
[h]**6:8** 1Sam 9:10
[i]**6:10** Ezr 7:23; Yer 29:7; Law 1:9; Mwa 8:21; 1Tim 2:1-2
[j]**6:11** Kum 21:22-23; Es 2:23; Ezr 7:26; Dan 2:5
[k]**6:12** Kut 20:24; Kum 12:11; 1Fal 9:3; 2Nya 7:16; Za 132:13

### *Jengo Linakamilika Na Kuwekwa Wakfu*

13 [a]Kwa sababu ya amri aliyotoa Mfalme
Dario, Tatenai mtawala wa Ng'ambo ya
Mto Frati na Shethar-Bozenai na wenzao
wakaitekeleza kwa bidii na kwa makini.
14 [b]Hivyo wazee wa Wayahudi waliendelea
kujenga na kustawi kutokana na mahubiri
ya manabii Hagai na Zekaria, mwana wa
Ido. Wakakamilisha ujenzi wa Hekalu
kulingana na agizo la Mungu wa Israeli
na amri ya Koreshi, Dario na Artashasta
wafalme wa Uajemi. 15 [c]Hekalu lilikamilika
siku ya kumi na mbili ya mwezi wa Adari,
ndio mwezi wa tatu, katika mwaka wa sita
wa utawala wa Mfalme Dario.

16 [d]Kisha watu wa Israeli: makuhani,
Walawi na wengine wote waliohamishwa,
wakaadhimisha kule kuwekwa wakfu
nyumba ya Mungu kwa shangwe. 17 [e]Kwa
ajili ya kuwekwa wakfu nyumba hii
ya Mungu walitoa mafahali mia moja,
kondoo dume mia mbili, wana-kondoo
mia nne, sadaka kwa ajili ya dhambi ya
Israeli yote walitoa mbuzi dume kumi na
wawili, mmoja kwa ajili ya kila kabila la
Israeli. 18 [f]Wakawaweka makuhani katika
nafasi zao na Walawi wakawekwa katika
makundi yao ya huduma kwa Mungu huko
Yerusalemu, kulingana na ilivyoandikwa
katika Kitabu cha Mose.

### *Pasaka*

19 [g]Katika siku ya kumi na nne ya mwezi
wa kwanza, waliorudi kutoka uhamishoni
wakaadhimisha Pasaka. 20 [h]Makuhani na
Walawi walikuwa wamekwisha kujitakasa
nao wamekuwa safi kwa kufuata kawaida
za ibada. Walawi wakachinja kondoo wa
Pasaka kwa ajili ya wana wa waliorudi
kutoka utumwani uhamishoni, kwa ajili
ya ndugu zao makuhani na wao wenyewe.
21 [i]Hivyo Waisraeli waliokuwa wamerudi
kutoka utumwani uhamishoni wakaila
Pasaka, pamoja na wale waliokuwa
wamejitenga na matendo ya unajisi wa
Mataifa ya jirani ili kumtafuta BWANA,
Mungu wa Israeli. 22 [j]Kwa muda wa siku
saba waliiadhimisha Sikukuu ya Mikate
Isiyotiwa Chachu kwa furaha, kwa sababu
BWANA alikuwa amewajaza furaha kwa
kubadilisha nia ya mfalme wa Ashuru
kwamba awasaidie ujenzi wa nyumba ya
Mungu, Mungu wa Israeli.

### *Ezra Awasili Yerusalemu*

7 [k]Baada ya mambo haya, wakati wa
utawala wa Artashasta mfalme wa
Uajemi, Ezra mwana wa Seraya, mwana
wa Azaria, mwana wa Hilkia, 2 [l]mwana
wa Shalumu, mwana wa Sadoki, mwana
wa Ahitubu, 3 mwana wa Amaria, mwana
wa Azaria, mwana wa Merayothi, 4 mwana
wa Zerahia, mwana wa Uzi, mwana wa
Buki, 5 mwana wa Abishua, mwana wa
Finehasi, mwana wa Eleazari, mwana wa
kuhani mkuu Aroni. 6 [m]Huyu Ezra alipanda
kutoka Babeli. Alikuwa mwalimu mwenye
ujuzi mzuri katika sheria ya Mose, ambayo
BWANA, Mungu wa Israeli, alikuwa ametoa.
Mfalme alikuwa amempa Ezra kila kitu
alichoomba, kwa maana BWANA Mungu
wake alikuwa pamoja naye. 7 [n]Pia baadhi ya
Waisraeli, wakiwemo makuhani, Walawi,
waimbaji, mabawabu na watumishi wa
Hekalu,[o] nao walikuja Yerusalemu mwaka
wa saba wa utawala wa Mfalme Artashasta.

8 Ezra aliwasili Yerusalemu mwezi wa
tano wa mwaka wa saba wa utawala wa
Mfalme Artashasta. 9 [p]Ezra alianza safari
yake kutoka Babeli tangu siku ya kwanza
ya mwezi wa kwanza, naye akawasili

---

[a]**6:13** Ay 5:12; Ezr 4:9; Za 9:16; 1Kor 3:19
[b]**6:14** Ezr 5:1; 7:1; Neh 2:1; Ezr 4:24
[c]**6:15** Zek 4:9
[d]**6:16** 1Fal 8:63; 2Nya 7:15; Yn 10:22
[e]**6:17** 2Sam 6:13; 1Nya 16:1-3; 2Nya 29:21; Hes 7:2-3; Ezr 8:25
[f]**6:18** 1Nya 24:1; 23:6; Hes 3:6-9; 8:9-11
[g]**6:19** Kut 12:11; Hes 28:16
[h]**6:20** 2Nya 30:15-17; 35:11; Kut 12:25; 2Nya 29:34
[i]**6:21** Kut 12:48; Za 93:5
[j]**6:22** Kut 12:17; Mit 21:1; Ezr 1:1
[k]**7:1** Ezr 4:7; Neh 2:1; 1Nya 6:14
[l]**7:2** 1Fal 2:35; Eze 40:46; Neh 11:11
[m]**7:6** Neh 12:36; Ezr 5:5; Isa 41:20; Mwa 32:28; Neh 1:10-11
[n]**7:7** Ezr 8:1; 2:43
[o]7 Yaani *Wanethini*
[p]**7:9** Neh 2:8

Yerusalemu siku ya kwanza ya mwezi wa
tano, kwa maana mkono wa neema wa
Mungu wake ulikuwa juu yake. 10 [a]Kwa
maana Ezra alikuwa amejitoa kwa moyo
wote kujifunza na kushika sheria ya BWANA
na kuwafundisha watu wa Israeli amri na
sheria zake.

*Barua Ya Ezra Kutoka Kwa Mfalme Artashasta*

11 Hii ni nakala ya barua ambayo Mfalme
Artashasta alikuwa amempa Ezra aliyekuwa
kuhani na mwalimu, mtu aliyeelimika
katika mambo yahusuyo maagizo na amri
za BWANA kwa Israeli.

12 [b]Artashasta, mfalme wa wafalme,

Kwa Ezra kuhani, mwalimu wa Sheria
ya Mungu wa mbinguni:

Salamu.

13 Sasa naamuru kwamba mtu yeyote
Mwisraeli katika ufalme wangu,
pamoja na makuhani na Walawi,
ambaye anataka kwenda Yerusalemu
pamoja nawe aweza kwenda.
14 [c]Unatumwa na mfalme na washauri
wake saba kuchunguza kuhusu Yuda
na Yerusalemu kulingana na Sheria
ya Mungu wako, iliyoko mkononi
mwako. 15 [d]Zaidi ya hayo, uchukue
pamoja nawe fedha na dhahabu
ambazo mfalme na washauri wake
wamempa Mungu wa Israeli kwa hiari,
Mungu ambaye maskani yake yako
Yerusalemu, 16 [e]pia fedha na dhahabu
zote unazoweza kupata kutoka jimbo
la Babeli, pamoja na sadaka za hiari
watakazotoa watu na makuhani kwa
ajili ya Hekalu la Mungu wao katika
Yerusalemu. 17 [f]Hakikisha kwamba
fedha hizi zimetumika kununua
mafahali, kondoo dume na
wana-kondoo pamoja na sadaka za
nafaka na sadaka za vinywaji, uvitoe
dhabihu juu ya madhabahu ya Hekalu
la Mungu wenu katika Yerusalemu.
18 Kisha wewe na Wayahudi
ndugu zako mnaweza kufanya lolote
linaloonekana jema sana kwa fedha
na dhahabu zilizosalia, kulingana na
mapenzi ya Mungu wenu. 19 [g]Uvitoe
kwa Mungu wa Yerusalemu vyombo
vyote ulivyokabidhiwa kwa ajili
ya ibada katika Hekalu la Mungu
wako. 20 [h]Kitu kingine chochote
kinachohitajika kwa ajili ya Hekalu
la Mungu wenu ambacho unatakiwa
kukitoa, waweza kukitoa kutoka
hazina ya mfalme.
21 [i]Mimi, Mfalme Artashasta, sasa
naagiza watunza hazina wote wa
Ng'ambo ya Mto Frati kutoa kwa bidii
chochote kwa Ezra kuhani na mwalimu
wa Sheria ya Mungu wa mbinguni
atakachohitaji kwenu, 22 talanta 100[j]
za fedha, ngano kori 100,[k] divai bathi
100,[l] mafuta ya zeituni bathi 100, na
chumvi kiasi chochote. 23 [m]Chochote
ambacho Mungu wa mbinguni
ameagiza, kifanyike kwa ukamilifu kwa
ajili ya Hekalu la Mungu wa mbinguni.
Kwa nini pawepo ghadhabu dhidi
ya utawala wa mfalme na wanawe?
24 [n]Pia ninyi fahamuni kuwa hamna
mamlaka ya kuwatoza kodi, ushuru
au ada makuhani, Walawi, waimbaji,
mabawabu, watumishi wa Hekalu au
wafanyakazi wengine kwenye nyumba
ya Mungu.
25 [o]Nawe Ezra, kufuatana na
hekima ya Mungu wenu uliyo nayo,

[a]**7:10** Kum 33:10; Neh 8:1-8; 2Tim 4:2; 1Sam 7:3; 2Nya 12:14; Za 10:18; 119:45; Mal 2:7
[b]**7:12** Eze 26:7; Dan 2:37; Ezr 4:10
[c]**7:14** Es 1:14
[d]**7:15** Kum 12:5; 1Nya 29:6; 2Nya 6:2; Za 135:21
[e]**7:16** Kut 3:22; Ezr 8:25; Zek 6:10; 1Nya 29:6
[f]**7:17** 2Fal 3:5; Hes 15:5-12; Kum 12:5-11
[g]**7:19** Ezr 5:14; Yer 27:22
[h]**7:20** Ezr 6:4; 1Kor 4:1-2
[i]**7:21** Ezr 4:16-20; 5:3-6
[j]22 Talanta 100 za fedha ni sawa na kilo 3,400.
[k]22 Kori 100 za ngano ni sawa na kilo 10,000.
[l]22 Bathi 100 za divai ni sawa na lita 2,000.
[m]**7:23** Ezr 6:10; Isa 60:12; Yer 12:14; Za 68:29; 1Tim 2:1-2
[n]**7:24** Ezr 4:13; 8:36
[o]**7:25** Kut 18:21-26; 16:18; Za 19:7; Kol 1:28; Kum 16:18; 2Nya 17:7; Mal 2:7; Mt 13:52

weka mahakimu na waamuzi wote wanaozifahamu sheria za Mungu wenu ili watoe haki kwa watu wote wa Ng'ambo ya Mto Frati. Nawe inakupasa umfundishe yeyote ambaye hazifahamu. 26 [a]Yeyote ambaye hataitii sheria ya Mungu wenu pia sheria ya mfalme, hakika lazima aadhibiwe kwa kuuawa, kuhamishwa, kunyang'anywa mali au kufungwa gerezani.

27 [b]Sifa ziwe kwa BWANA, Mungu wa baba zetu, Mungu ambaye kwa njia hii ameweka ndani ya moyo wa mfalme kuipa heshima nyumba ya BWANA iliyoko Yerusalemu, kwa namna hii 28 [cd]ambaye ameniongezea kibali chake mbele ya mfalme, washauri wake na maafisa wote wa mfalme wenye uwezo. Kwa kuwa mkono wa BWANA Mungu wangu ulikuwa pamoja nami, nilijipa moyo nikakusanya watu walio viongozi kutoka Israeli wakwee pamoja nami.

*Orodha Ya Viongozi Wa Jamaa Waliorudi Na Ezra*

8 [e]Hawa ndio viongozi wa jamaa pamoja na wale walioandikwa ambao walikuja pamoja nami kutoka Babeli wakati wa utawala wa Mfalme Artashasta:

2 [f]wa wazao wa Finehasi, alikuwa Gershoni;
wa wazao wa Ithamari, alikuwa Danieli;
wa wazao wa Daudi, alikuwa Hatushi 3 [g]wa wazao wa Shekania;

wa wazao wa Paroshi, alikuwa Zekaria, na watu 150 walioandikishwa pamoja naye;
4 [h]wa wazao wa Pahath-Moabu, alikuwa Eliehoenai mwana wa Zerahia na wanaume 200 pamoja naye;
5 wa wazao wa Zatu, alikuwa Shekania mwana wa Yahazieli na wanaume 300 pamoja naye;
6 [i]wa wazao wa Adini, alikuwa Ebedi mwana wa Yonathani na wanaume 50 pamoja naye;
7 wa wazao wa Elamu, alikuwa Yeshaya mwana wa Athalia, na wanaume 70 pamoja naye;
8 wa wazao wa Shefatia, alikuwa Zebadia mwana wa Mikaeli na wanaume 80 pamoja naye;
9 wa wazao wa Yoabu, alikuwa Obadia mwana wa Yehieli na wanaume 218 pamoja naye;
10 wa wazao wa Bani, alikuwa Shelomithi mwana wa Yosifia na wanaume 160 pamoja naye;
11 wa wazao wa Bebai, alikuwa Zekaria mwana wa Bebai na wanaume 28 pamoja naye;
12 wa wazao wa Azgadi, alikuwa Yohanani mwana wa Hakatani na wanaume 110 pamoja naye;
13 [j]wa wazao wa Adonikamu, hawa walikuwa wa mwisho ambao majina yao ni Elifeleti, Yeueli, Shemaya na wanaume 60 pamoja nao;
14 wa wazao wa Bigwai, walikuwa Uthai na Zakuri na wanaume 70 pamoja nao.

*Kurudi Yerusalemu*

15 [k]Niliwakusanya kwenye mto utiririkao
kuelekea Ahava, nasi tukapiga kambi pale
siku tatu. Wakati nilipokagua kati ya
watu na makuhani, sikuwapata Walawi.
16 Basi niliwaita Eliezeri, Arieli, Shemaya,
Elnathani, Yaribu, Elnathani, Nathani,
Zekaria na Meshulamu waliokuwa
viongozi na Yoyaribu na Elnathani
waliokuwa wasomi, 17 [l]nikawatuma kwa

[a]**7:26** Eze 6:11
[b]**7:27** Ezr 6:22; 1Nya 29:12; Neh 2:12; 2Kor 8:16; Flp 4:10; Mit 16:7
[c]**7:28** 2Fal 25:28; Ezr 5:5; 9:9; Neh 1:11
[d]**7:28** Neh 8:7; Rum 8:28; Mit 3:6; Law 10:10-11; 2Nya 30:22
[e]**8:1** Ezr 7:7
[f]**8:2** 1Nya 3:22
[g]**8:3** 1Nya 3:22; Ezr 2:3
[h]**8:4** Ezr 2:6
[i]**8:6** Ezr 2:15; Neh 7:20
[j]**8:13** Ezr 2:13
[k]**8:15** Ezr 2:40; 7:7; Mdo 16:13; 20:28; Za 137:1; Mit 27:23; Ebr 13:17; Ezr 7:7; Hes 8:1
[l]**8:17** Ezr 2:43

Ido kiongozi huko Kasifia. Niliwaambia
watakayomwambia Ido na ndugu zake,
watumishi wa Hekalu[a] huko Kasifia, ili
waweze kutuletea wahudumu kwa ajili ya
nyumba ya Mungu wetu. 18 [b]Kwa sababu
mkono wa neema wa Mungu wetu ulikuwa
juu yetu, walituletea Sherebia, mtu mwenye
uwezo kutoka wazao wa Mahli mwana
wa Lawi, mwana wa Israeli, na wana wa
Sherebia pamoja na ndugu zao wanaume
kumi na wanane. 19 Naye Hashabia, pamoja
na Yeshaya kutoka wazao wa Merari na
ndugu zake na wapwa wake wanaume
ishirini. 20 [c]Vilevile walileta watumishi wa
Hekalu 220, kikundi ambacho Daudi na
maafisa walikuwa wamekiweka kusaidia
Walawi. Wote walikuwa wameorodheshwa
kwa majina.

21 [de]Kando ya Mto Ahava, hapo nilitangaza
kufunga, ili tujinyenyekeshe mbele za
Mungu wetu na kumwomba kwa ajili ya
kutujalia safari ya amani sisi na watoto
wetu, pamoja na mali zetu zote. 22 [f]Niliona
aibu kumwomba mfalme askari na wapanda
farasi wa kutulinda njiani kutokana na adui
zetu, kwa sababu tulikwisha kumwambia
mfalme, "Mkono wa neema wa Mungu
wetu uko juu ya kila mmoja anayemtafuta,
lakini hasira yake kubwa ni dhidi ya wote
wamwachao." 23 [g]Kwa hiyo tulifunga na
kumwomba Mungu wetu kuhusu jambo
hili, naye akajibu maombi yetu.

24 Kisha niliwatenga viongozi wa
makuhani kumi na wawili, pamoja na
Sherebia, Hashabia na ndugu zao kumi,
25 [h]nami nikawapimia fedha, dhahabu na
vifaa ambavyo mfalme, washauri wake,
maafisa wake na Israeli wote waliokuwepo
walikuwa wamevitoa sadaka kwa ajili ya
nyumba ya Mungu wetu. 26 Niliwapimia
talanta 650[i] za fedha, vifaa vingine vya
fedha vya uzito wa talanta mia moja,[j]
talanta mia moja za dhahabu, 27 mabakuli
ishirini ya dhahabu ya thamani ya darkoni
elfu moja,[k] na vyombo viwili vya shaba
iliyosuguliwa, ya thamani kama dhahabu.

28 [l]Niliwaambia, "Ninyi pamoja na
vyombo hivi ni wakfu kwa Bwana. Fedha
na dhahabu ni sadaka ya hiari kwa Bwana,
Mungu wa baba zenu. 29 [m]Vilindeni kwa
uangalifu mpaka mtakapovipima ndani
ya vyumba vya nyumba ya Bwana katika
Yerusalemu mbele ya makuhani, viongozi
na Walawi pamoja na wakuu wa jamaa
za Israeli." 30 Ndipo makuhani na Walawi
wakapokea fedha, dhahabu na vyombo
vilivyowekwa wakfu ambavyo vilipimwa
na kupelekwa katika nyumba ya Mungu
wetu mjini Yerusalemu.

31 [n]Tulianza safari kutoka Mto Ahava
kwenda Yerusalemu kwenye siku ya kumi
na mbili ya mwezi wa kwanza. Mkono wa
Mungu wetu ulikuwa juu yetu, naye njiani
alitulinda dhidi ya adui na wanyang'anyi.
32 [o]Kwa hiyo tuliwasili Yerusalemu ambapo
tulipumzika kwa siku tatu.

33 [p]Katika siku ya nne, ndani ya nyumba
ya Mungu wetu, tulipima fedha, dhahabu na
vyombo vilivyowekwa wakfu, tukakabidhi
mikononi mwa kuhani Meremothi mwana
wa Uria. Eleazari mwana wa Finehasi
alikuwa pamoja naye, pia walikuwako
Walawi wawili, Yozabadi mwana wa
Yeshua na Noadia mwana wa Binui. 34 Kila
kitu kilihesabiwa kwa idadi na kupimwa
kwa uzito, nao uzito wote uliandikwa
wakati ule.

---

[a]17 Yaani *Wanethini*
[b]**8:18** Ezr 5:5
[c]**8:20** 1Nya 9:2; Ezr 2:43
[d]**8:21** 2Nya 9:2; Ezr 2:43
[e]**8:21** 2Nya 20:3; Za 27:11; Law 16:29; Za 5:8; 2Nya 20:3; Law 16:29; Isa 58:3-5
[f]**8:22** Neh 2:9; Yer 41:16; Kum 31:17; 2Nya 15:2; 1Kor 9:15; 1Nya 28:9; Ezr 7:6-9; Za 33:18-19; Isa 3:10; Rum 8:28; 1Pet 3:12; Za 34:16; 2Nya 15:2
[g]**8:23** 2Nya 33:13; Kum 4:29; Mdo 14:23; 1Nya 5:20; Isa 19:22; Yer 29:12-13
[h]**8:25** Ezr 7:15-16
[i]26 Talanta 650 za fedha ni sawa na tani 25.
[j]26 Talanta 100 za fedha ni sawa na tani 3.75.
[k]27 Darkoni 1,000 ni sawa na kilo 8.5.
[l]**8:28** Kum 33:8; Law 21:6; 22:2-3; 2Nya 24:14; Hes 4:4; Isa 52:11; 1Nya 23:28
[m]**8:29** 1Nya 26:20-26; Lk 12:38-39
[n]**8:31** Ay 5:19-24; Isa 41:10-14; Ezr 7:6-7, 28
[o]**8:32** Mwa 40:13; Neh 2:11; Isa 56:6; 14:1
[p]**8:33** Neh 3:3, 21-24

35 [a]Kisha mateka waliokuwa wamerudi kutoka utumwani wakatoa sadaka za kuteketezwa kwa moto kwa Mungu wa Israeli: mafahali kumi na wawili kwa ajili ya Israeli wote, kondoo dume tisini na sita, wana-kondoo sabini na saba na mbuzi dume kumi na wawili kuwa sadaka ya dhambi. Hii yote ilikuwa sadaka ya kuteketezwa kwa moto kwa BWANA.
36 [b]Pia walikabidhi manaibu wa mfalme na watawala wa Ng'ambo ya Mto Frati maagizo ya mfalme, ambao baadaye walitoa msaada kwa watu na kwa nyumba ya Mungu.

*Maombi Ya Ezra Kuhusu Kuoa Wake Wa Kigeni*

9 [c]Baada ya mambo haya kutendeka, viongozi walinijia na kusema, "Watu wa Israeli, wakiwemo makuhani na Walawi, hawakujitenga na majirani zao katika kufanya machukizo, kama yale ya Wakanaani, Wahiti, Waperizi, Wayebusi, Waamoni, Wamoabu, Wamisri na Waamori.
2 [d]Wamewaoa baadhi ya binti zao kuwa wake zao na wake za wana wao, nao wamechanganya taifa takatifu na watu waliowazunguka. Nao viongozi na maafisa wamekuwa mstari wa mbele katika njia hii potovu."
3 [e]Niliposikia jambo hili nilirarua koti langu na joho langu, nikazing'oa nywele za kichwa changu na ndevu zangu na kuketi nikishangaa.
4 [fg]Kisha kila mmoja aliyetetemeshwa na maneno ya Mungu wa Israeli alikusanyika kunizunguka kwa sababu ya upotovu huu wa hao watu waliorudi kutoka utumwani. Nami niliketi pale nikishangaa mpaka wakati wa dhabihu ya jioni.
5 [h]Ndipo wakati wa kutoa dhabihu ya jioni nikainuka kutoka kujidhili kwangu nikiwa na koti na joho langu lililoraruka, nikapiga magoti mikono yangu ikiwa imeinuliwa kwa BWANA Mungu wangu.
6 [i]Nami nikaomba:

"Ee Mungu wangu, natahayari na kuona aibu kukuinulia uso wangu Mungu wangu, kwa sababu dhambi zetu zimejikusanya hata kupita juu ya vichwa vyetu na hatia yetu imefika mbinguni.
7 [j]Tokea siku za babu zetu mpaka sasa, hatia yetu imekuwa kubwa. Kwa sababu ya dhambi zetu, sisi na wafalme wetu na makuhani wetu tumekabiliwa na vita, utumwa, kutekwa na kudhiliwa katika mikono ya wafalme wa kigeni, kama ilivyo leo.
8 [k]"Lakini sasa, kwa muda mfupi, BWANA Mungu wetu amekuwa na neema kwa kutuachia mabaki na kutupa mahali imara katika mahali pake patakatifu, hivyo Mungu wetu atupa mwanga machoni petu na unafuu katika utumwa wetu.
9 [l]Ingawa tu watumwa, Mungu wetu hajatuacha katika kufungwa kwetu. Ametuonyesha huruma mbele ya wafalme wa Uajemi: Ametujalia maisha mapya kwa kujenga upya nyumba ya Mungu wetu na kukarabati magofu yake, naye ametupa ukuta wa ulinzi katika Yuda na Yerusalemu.
10 [m]"Lakini sasa, Ee Mungu wetu, tunaweza kusema nini baada ya hili? Kwa maana tumedharau maagizo
11 [n]uliyoyatoa kupitia watumishi wako manabii uliposema: 'Nchi mnayoiingia kuimiliki ni nchi iliyochafuliwa na uovu wa watu wake. Kwa matendo yao ya machukizo wameijaza nchi kwa unajisi wao kutoka mwisho mmoja hadi

---

[a]**8:35** Law 1:3; 2Nya 29:21, 24; 30:24; Ezr 6:17
[b]**8:36** Ezr 7:21-24; Zek 8:1-23; Es 9:3
[c]**9:1** Neh 9:2; Mwa 19:38; Kum 20:17; Amu 3:5; Kum 12:30
[d]**9:2** Law 27:30; Ezr 10:2; 2Kor 6:14; Kut 22:31; Kum 7:3
[e]**9:3** Isa 15:2; Za 143:4
[f]**9:4** Za 119:120; Isa 66:2-5
[g]**9:4** Ezr 10:3; Kut 29:39
[h]**9:5** Kut 9:29; 29:41
[i]**9:6** Ufu 18:5; Dan 9:7; Isa 59:12
[j]**9:7** 2Nya 29:6; Eze 21:1-32; Kum 28:36-64; Za 106:6; 2Nya 19:2; Mwa 18:19
[k]**9:8** Isa 33:2; Za 13:3; Mhu 12:11; Mwa 45:7; Isa 22:23; Za 19:8
[l]**9:9** Neh 9:36; Kut 1:14; 2Fal 25:28; Zek 1:16-17; Ezr 7:28
[m]**9:10** Kum 11:8; Isa 1:19-20
[n]**9:11** Law 18:25-28; Kum 18:9; 1Fal 14:24

mwingine. 12 [a][b]Kwa hiyo, msiwaoze
binti zenu kwa wana wao wala binti zao
kwa wana wenu. Msitafute mkataba
wa urafiki nao kwa wakati wowote.
Ndipo mtakapofanikiwa na kula mema
ya nchi na kuwaachia watoto wenu
nchi hiyo kama urithi wao wa milele.'
13 [c]"Yale yaliyotupata ni matokeo
ya matendo yetu mabaya, pia hatia
yetu kubwa. Hata hivyo, wewe Mungu
wetu, umetuadhibu kidogo kuliko
dhambi zetu zilivyostahili na umetupa
mabaki kama haya. 14 [d]Je, tutavunja
maagizo yako tena na kuoana na watu
ambao hufanya mambo ya machukizo?
Je, hutakuwa na hasira ya kutosha juu
yetu na kutuangamiza, bila kutuachia
mabaki wala atakayenusurika? 15 [e]Ee
BWANA, Mungu wa Israeli, wewe ni
mwenye haki! Leo hii tumeachwa
kama mabaki. Tupo hapa mbele zako
na hatia yetu, ingawa katika hali hii
hakuna hata mmoja wetu anayeweza
kusimama mbele zako."

*Toba Ya Watu*

10 [f]Wakati Ezra alipokuwa anaomba na
kuungama, huku akilia na kujitupa
chini mbele ya nyumba ya Mungu, umati
mkubwa wa Waisraeli, wanaume, wanawake
na watoto walikusanyika kumzunguka. Nao
pia wakalia sana. 2 [g]Kisha Shekania mwana
wa Yehieli, mmoja wa wazao wa Elamu,
akamwambia Ezra, "Tumekosa uaminifu
kwa Mungu wetu kwa kuoa wanawake wa
kigeni kutoka mataifa yanayotuzunguka.
Lakini pamoja na hili, bado liko tumaini
kwa ajili ya Israeli. 3 [h]Sasa na tufanye agano
mbele za Mungu wetu kuwafukuza hawa
wanawake wote pamoja na watoto wao,
kulingana na maonyo ya bwana wangu
pamoja na wale ambao wanaogopa amri za
Mungu wetu. Hili na lifanyike sawasawa na
hii Sheria. 4 [i]Inuka, suala hili lipo mikononi
mwako. Sisi tutaungana nawe, uwe na
ujasiri ukatende hili."
5 [j]Basi Ezra akainuka na kuwaapisha
makuhani viongozi, Walawi na Israeli yote
kufanya lile lililokuwa limependekezwa.
Nao wakaapa. 6 [k]Ndipo Ezra akaondoka
hapo mbele ya nyumba ya Mungu akaenda
kwenye chumba cha Yehohanani mwana
wa Eliashibu. Wakati alipokuwa hapo,
hakula chakula wala hakunywa maji, kwa
sababu aliendelea kuomboleza kuhusu
kukosa uaminifu kwa watu wa uhamishoni.
7 Ndipo lilipotolewa tangazo Yuda yote
na Yerusalemu kwa watu wote waliokuwa
uhamishoni kukusanyika Yerusalemu.
8 [l]Yeyote ambaye hangejitokeza kwa
muda wa siku tatu angepoteza mali yake
yote, kulingana na uamuzi wa maafisa na
wazee, naye mtu huyo angefukuzwa kutoka
kusanyiko la watu waliokuwa uhamishoni.

9 [m]Katika muda wa siku tatu, watu
wote wa Yuda na Benyamini wakawa
wamekusanyika huko Yerusalemu. Kwenye
siku ya ishirini ya mwezi wa tisa, watu wote
walikuwa wameketi ndani ya uwanja mbele
ya nyumba ya Mungu, wakiwa na majonzi
mno kwa tukio hilo na kwa sababu ya mvua
kubwa. 10 Ndipo Kuhani Ezra aliposimama
akawaambia, "Mmekosa uaminifu, mmeoa
wanawake wa kigeni, mkaongezea hatia ya
Israeli. 11 [n]Sasa tubuni kwa BWANA, Mungu
wa baba zenu mkafanye mapenzi yake.
Jitengeni na mataifa wanaowazunguka na
wake zenu wa kigeni."
12 [o]Kusanyiko lote likajibu kwa sauti
kubwa: "Uko sawa kabisa! Ni lazima

[a]**9:12** Kut 34:15; Kum 7:3
[b]**9:12** Mit 13:22; Kut 23:32-33; Amu 2:2; 2Pet 2:20; 2Kor 6:14
[c]**9:13** Ay 15:5; Za 103:10
[d]**9:14** Kum 9:8-14; Neh 13:27; Yn 5:14
[e]**9:15** Neh 9:33; Za 51:4; Rum 3:19; Isa 24:16; 1Fal 8:47; Dan 9:14; Za 130:3
[f]**10:1** 2Nya 20:9; Dan 9:20
[g]**10:2** Ezr 9:2; Kut 34:13; Neh 13:27; Kum 30:8-10
[h]**10:3** 2Fal 11:17; 2Nya 34:31; Kut 34:16; Kum 7:2-3; Ezr 9:4; Za 119:53, 120; Isa 66:2
[i]**10:4** 1Nya 28:10; Isa 35:3-4
[j]**10:5** Neh 5:12; 13:25
[k]**10:6** Kum 9:18; Yn 3:7; Za 102:4
[l]**10:8** Law 27:28; Yos 6:19
[m]**10:9** 1Sam 12:18; Ezr 1:5
[n]**10:11** Kum 24:1; Mit 28:13; Mal 2:10-16; Yer 3:13; Isa 1:16-17; Rum 12:2
[o]**10:12** Yos 6:5

tufanye kama unavyosema. 13 Lakini hapa
pana watu wengi na ni wakati wa mvua,
hivyo hatuwezi kusimama nje. Hata hivyo,
shauri hili haliwezi kumalizika kwa siku
moja au mbili, kwa sababu tumefanya
dhambi kubwa katika jambo hili. 14 [a]Maafisa
wetu na wafanye kwa niaba ya kusanyiko
lote. Kisha kila mmoja katika miji yetu
ambaye ameoa mwanamke wa kigeni aje
kwa wakati uliopangwa, akiwa pamoja
na wazee na waamuzi wa kila mji, hadi
hasira kali ya Mungu wetu katika shauri
hili itakapoondolewa kwetu." 15 [b]Yonathani
mwana wa Asaheli na Yazeya mwana wa
Tikwa peke yao, wakiungwa mkono na
Meshulamu na Shabethai Mlawi, ndio
waliopinga jambo hili.

16 Basi watu wa uhamishoni wakafanya
kama ilivyokuwa imependekezwa. Kuhani
Ezra akachagua wanaume waliokuwa
viongozi wa jamaa, mmoja kutoka
kila mgawanyo wa jamaa, nao wote
wakachaguliwa kwa majina. Katika siku
ya kwanza ya mwezi wa kumi waliketi
kuchunguza mashauri hayo. 17 Katika siku
ya kwanza ya mwezi wa kwanza wakawa
wamemaliza kushughulikia wanaume wote
waliokuwa wameoa wanawake wa kigeni.

*Wenye Hatia Ya Kuoa Wake Wa Kigeni*

18 [c]Miongoni mwa wazao wa
makuhani, wafuatao walikuwa
wameoa wanawake wa kigeni:

Kutoka wazao wa Yeshua mwana
wa Yosadaki na ndugu zake:
Maaseya, Eliezeri, Yaribu na
Gedalia. 19 [d](Wote walitoa nadhiri
kwa kuandika kwa mikono yao
kuwafukuza wake zao, kwa hatia
yao, kila mmoja akatoa kondoo
dume kutoka kundini mwake
kama sadaka ya hatia.)

20 [e]Kutoka wazao wa Imeri:
Hanani na Zebadia.
21 [f]Kutoka wazao wa Harimu:
Maaseya, Eliya, Shemaya, Yehieli
na Uzia.
22 [g]Kutoka wazao wa Pashuri:
Elioenai, Maaseya, Ishmaeli,
Nethaneli, Yozabadi na Elasa.

23 [h]Miongoni mwa Walawi:
Yozabadi, Shimei, Kelaya (ndiye
Kelita), Pethahia, Yuda na Eliezeri.
24 [i]Kutoka waimbaji:
Eliashibu.
Kutoka mabawabu:
Shalumu, Telemu na Uri.

25 [j]Miongoni mwa Waisraeli wengine:

Kutoka wazao wa Paroshi:
Ramia, Izia, Malkiya, Miyamini,
Eleazari, Malkiya na Benaya.
26 Kutoka wazao wa Elamu:
Matania, Zekaria, Yehieli, Abdi,
Yeremothi na Eliya.
27 Kutoka wazao wa Zatu:
Elioenai, Eliashibu, Matania,
Yeremothi, Zabadi na Aziza.
28 Kutoka uzao wa Bebai:
Yehohanani, Hanania, Zabai na
Athlai.
29 Kutoka wazao wa Bani:
Meshulamu, Maluki, Adaya,
Yashubu, Sheali na Yeremothi.
30 Kutoka wazao wa Pahath-Moabu:
Adna, Kelali, Benaya, Maaseya,
Matania, Bezaleli, Binui na
Manase.
31 Kutoka wazao wa Harimu:
Eliezeri, Ishiya, Malkiya, Shemaya,
Shimeoni, 32 Benyamini, Maluki,
na Shemaria.
33 Kutoka wazao wa Hashumu:
Matenai, Matata, Zabadi, Elifeleti,
Yeremai, Manase na Shimei.
34 Kutoka wazao wa Bani:

---

[a]**10:14** Kum 16:18; Hes 25:4; 2Nya 30:8; 2Fal 23:26; 2Nya 28:11-13; 29:10; 30:8; Za 78:38; Isa 12:1
[b]**10:15** Neh 11:16
[c]**10:18** Ezr 5:2; Amu 3:6; Zek 6:1
[d]**10:19** 2Fal 10:15; Law 5:15; 6:4-6; 1Nya 29:24; 2Nya 30:8; Gal 2:9; Mit 22:26
[e]**10:20** 1Nya 24:14
[f]**10:21** 1Nya 24:8
[g]**10:22** 1Nya 9:12
[h]**10:23** Neh 8:7; 9:4
[i]**10:24** Neh 3:1; 12:10
[j]**10:25** Ezr 3:2; 8:3; Neh 7:13

Maadai, Amramu, Ueli, 35 Benaya,
Bedeya, Keluhi, 36 Vania,
Meremothi, Eliashibu, 37 Matania,
Matenai na Yaasu.
38 Kutoka wazao wa Binui:
Shimei, 39 Shelemia, Nathani,
Adaya, 40 Maknadebai, Shashai,
Sharai, 41 Azareli, Shelemia,
Shemaria, 42 Shalumu, Amaria na
Yosefu.
43 [a]Kutoka wazao wa Nebo:
Yeieli, Matithia, Zabadi, Zebina,
Yadai, Yoeli na Benaya.

44 [b]Hawa wote walikuwa wameoa
wanawake wa kigeni, na baadhi yao
walikuwa wamezaa nao watoto.

---

[a]**10:43** Ezr 2:29; Hes 32:38
[b]**10:44** Mwa 6:2-5; Kut 23:2; Kum 7:3

# NEHEMIA

*Maombi Ya Nehemia*

1 [a]Maneno ya Nehemia mwana wa Hakalia:

Katika mwezi wa Kisleu[b] katika mwaka
wa ishirini, wakati nilikuwa ngomeni katika
jumba la kifalme la Shushani, 2 [c]Hanani,
mmoja wa ndugu zangu, alikuja kutoka
Yuda akiwa na watu wengine, nami
nikawauliza kuhusu mabaki ya Wayahudi
wale walionusurika kwenda uhamishoni na
pia kuhusu Yerusalemu.
3 [d]Wakaniambia, "Wale walionusurika
kwenda uhamishoni, wale ambao wamerudi
kwenye lile jimbo, wako katika taabu kubwa
na aibu. Ukuta wa Yerusalemu umebomoka,
na malango yake yamechomwa moto."
4 [e]Niliposikia mambo haya, niliketi,
nikalia. Kwa siku kadhaa niliomboleza na
kufunga na kuomba mbele za Mungu wa
mbinguni. 5 [f]Kisha nikasema:

> "Ee Bwana, Mungu wa mbinguni,
> mkuu na mwenye kuogofya, ambaye
> hulishika agano lake la upendo na wale
> wampendao na kutii amri zake, 6 [g]tega
> masikio yako, na ufungue macho
> yako, ili usikie maombi ya mtumishi
> wako anayoomba mbele yako usiku na
> mchana kwa ajili ya watumishi wako,
> watu wa Israeli. Ninaungama dhambi
> zetu sisi Waisraeli, pamoja na zangu na
> za nyumba ya baba yangu, tulizotenda
> dhidi yako. 7 [h]Tumetenda uovu sana
> mbele zako. Hatukutii amri, maagizo
> na sheria ulizompa Mose mtumishi
> wako.
> 8 [i]"Kumbuka agizo ulilompa Mose
> mtumishi wako, ukisema, 'Kama
> mkikosa uaminifu, nitawatawanya
> miongoni mwa mataifa, 9 [j]lakini
> mkinirudia na kutii amri zangu,
> ndipo hata kama watu wenu walio
> uhamishoni wako mbali sana katika
> miisho ya dunia, nitawakusanya
> kutoka huko na kuwaleta mahali
> ambapo nimepachagua kuwa makao
> kwa ajili ya Jina langu.'
> 10 [k]"Hawa ni watumishi wako na
> watu wako, uliowakomboa kwa nguvu
> zako kuu na mkono wako wenye
> nguvu. 11 [l]Ee Bwana, tega sikio lako
> na usikie maombi ya huyu mtumishi
> wako, na maombi ya watumishi
> wako wanaofurahia kuliheshimu Jina
> lako. Nipe leo, mimi mtumishi wako,
> mafanikio kwa kunipa kibali mbele ya
> mtu huyu."

Kwa maana nilikuwa mnyweshaji wa
mfalme.

*Artashasta Amtuma Nehemia Yerusalemu*

2 [m]Katika mwezi wa Nisani[n] mwaka
wa ishirini wa utawala wa Mfalme
Artashasta, wakati divai ilipoletwa kwake,
niliichukua na kumpa mfalme. Sikuwahi
kuonekana mwenye huzuni mbele yake
kabla ya hapo. 2 [o]Basi mfalme akaniuliza,
"Kwa nini uso wako unaonekana una
huzuni wakati wewe si mgonjwa? Jambo
hili si kitu kingine bali ni huzuni ya moyo."

---

[a]**1:1** Neh 10:1; Ezr 7:8; Zek 7:1; Dan 8:2; Neh 2:1; Es 1:2
[b]1 Kisleu ni mwezi wa tisa katika kalenda ya Kiyahudi; katika kalenda yetu ni Novemba/Desemba (ona pia Zekaria 7:1).
[c]**1:2** Neh 7:2; 2Fal 21:4; Neh 7:6; Yer 52:28
[d]**1:3** Law 26:31; Mao 2:9; Yer 5:10; Law 26:31; 2Fal 25:10; Neh 2:3, 13, 17; Isa 22:9
[e]**1:4** Za 137:1; 2Nya 20:3; Ezr 9:4; Dan 9:3
[f]**1:5** Kum 7:21; Neh 4:14; Kum 7:9; 1Fal 8:23; Ebr 6:13-18
[g]**1:6** 2Nya 7:15; 1Fal 8:30; 2Nya 6:40; 1Fal 8:47
[h]**1:7** Kum 28:14-15; Za 106:6
[i]**1:8** Mwa 8:1; Law 26:33; Kum 4:25
[j]**1:9** Kum 30:4; Eze 20:34-38; Mik 2:12
[k]**1:10** Kum 9:29; Isa 51:9-11; Dan 9:15
[l]**1:11** 2Nya 6:40; Mwa 40:1; 32:11; Isa 26:8
[m]**2:1** Ezr 4:7; 7:1
[n]1 Nisani (Abibu) ni mwezi wa kwanza katika kalenda ya Kiyunani; katika kalenda yetu ni Machi/Aprili.
[o]**2:2** Mit 15:13

Niliogopa sana, 3 [a]lakini nikamwambia
mfalme, “Mfalme na aishi milele! Kwa
nini uso wangu usiwe na huzuni wakati
mji walipozikwa baba zangu umebaki
magofu, na malango yake yameteketezwa
kwa moto?”
4 [b]Mfalme akaniambia, “Je, haja yako ni
gani?”

Ndipo nikaomba kwa Mungu wa
mbinguni, 5 na nikamjibu mfalme, “Kama
ikimpendeza mfalme, na kama mtumishi
wako amepata kibali machoni pake,
anitume kule mji wa Yuda, mahali baba
zangu walipozikwa, ili niweze kuujenga
upya.”
6 [c]Kisha mfalme, na malkia akiwa ameketi
karibu naye, akaniuliza, “Safari yako
itachukua muda gani, nawe utarudi lini?”
Ilimpendeza mfalme kunituma, kwa hiyo
nikapanga muda.
7 [d]Pia nikamwambia, “Kama ikimpendeza
mfalme, naomba nipewe barua kwa
watawala wa Ng’ambo ya Frati, ili wanipe
ulinzi mpaka nifike Yuda. 8 [e]Naomba
nipewe barua nipeleke kwa Asafu, mtunzaji
wa msitu wa mfalme, ili anipe miti ya
kutengeneza boriti kwa ajili ya malango
ya ngome ya Hekalu, na ukuta wa mji, na
makao yangu nitakapoishi.” Kwa kuwa
mkono wenye neema wa Mungu wangu
ulikuwa juu yangu, mfalme akanijalia
ombi langu. 9 [f]Basi nilienda kwa watawala
wa Ng’ambo ya Frati na kuwapa barua za
mfalme. Pia mfalme alikuwa ametuma
maafisa wa jeshi na askari wapanda farasi
pamoja nami.
10 [g]Sanbalati Mhoroni na Tobia afisa
Mwamoni waliposikia juu ya jambo hili,
waliudhika sana kwamba amekuja mtu
kuinua ustawi wa Waisraeli.

*Nehemia Akagua Kuta Za Yerusalemu*

11 [h]Nilienda Yerusalemu, na baada ya
kukaa huko siku tatu, 12 nikaondoka wakati
wa usiku pamoja na watu wachache.
Sikuwa nimemwambia mtu yeyote kile
ambacho Mungu wangu alikuwa ameweka
moyoni mwangu kufanya kwa ajili ya
Yerusalemu. Hapakuwepo na mnyama
yeyote pamoja nami isipokuwa yule
niliyekuwa nimempanda.
13 [i]Nikatoka nje usiku kupitia Lango
la Bondeni, kuelekea Kisima cha Joka
na Lango la Samadi, nikikagua kuta za
Yerusalemu zilizokuwa zimebomolewa, na
malango yake yaliyokuwa yameteketezwa
kwa moto. 14 [j]Kisha nikaelekea mpaka
Lango la Chemchemi na Bwawa la Mfalme,
lakini hapakuwepo nafasi ya kutosha kwa
ajili ya mnyama wangu kupita, 15 [k]kwa
hiyo nikapandia bondeni usiku nikikagua
ukuta. Mwishoni nikarudi na kuingia
tena kupitia Lango la Bondeni. 16 Maafisa
hawakujua nilikokwenda wala nilichokuwa
nikifanya, kwa sababu mpaka sasa nilikuwa
bado sijasema lolote kwa Wayahudi, wala
makuhani, wala wakuu, wala maafisa, wala
mtu yeyote ambaye angefanya kazi.
17 [l]Ndipo nilipowaambia, “Mnaona taabu
tuliyo nayo: Yerusalemu imebaki magofu na
malango yake yameteketezwa kwa moto.
Njooni tujenge upya ukuta wa Yerusalemu,
nasi hatutakuwa tena katika aibu hii.” 18 [m]Pia
niliwaambia kuhusu mkono wenye neema
wa Mungu wangu uliokuwa juu yangu, na
kile mfalme alichokuwa ameniambia.

Wakajibu, “Haya! Tuanze kujenga tena.”
Kwa hiyo wakaanza kazi hii njema.
19 [n]Lakini Sanbalati Mhoroni, Tobia
afisa Mwamoni, na Geshemu Mwarabu
waliposikia kuhusu jambo hili,
walitudhihaki na kutucheka. Wakauliza,

---

[a]**2:3** 1Fal 1:13; Dan 3:9; 5:10; Za 137:6
[b]**2:4** 1Sam 1:13; Mit 3:6
[c]**2:6** Neh 5:14; 13:6
[d]**2:7** Ezr 8:36
[e]**2:8** Neh 3:7; Ezr 7:6; Neh 7:2; Mdo 7:10
[f]**2:9** Ezr 8:22
[g]**2:10** Neh 2:10; 4:1, 7; 6:1-2, 5, 12, 14; 13:28; 4:3; 13:4-7; Es 10:3
[h]**2:11** Mwa 40:13
[i]**2:13** 2Nya 26:9; Neh 12:31; 3:13
[j]**2:14** Neh 12:37; 2Fal 18:17; 20:20
[k]**2:15** 2Sam 15:23; Yer 31:40; Yn 18:1
[l]**2:17** Za 102:16; Isa 30:13; 58:12; Eze 5:14; Neh 1:3
[m]**2:18** Ezr 5:5; 2Sam 2:7
[n]**2:19** Neh 6:1-6; Za 44:13-16

“Ni nini hiki mnachokifanya? Je, mnaasi
dhidi ya mfalme?”
20 [a]Nikawajibu kwa kusema, “Mungu wa
mbinguni atatufanikisha. Sisi watumishi
wake tutaanza kujenga upya, lakini kwenu
ninyi, hamna sehemu wala dai lolote wala
kumbukumbu la haki katika Yerusalemu.”

*Wajenzi Wa Ukuta*

3 [b]Eliashibu kuhani mkuu na makuhani
wenzake walikwenda kufanya kazi na
kulijenga upya Lango la Kondoo. Waliliweka
wakfu na kuweka milango mahali pake,
wakajenga hadi kufikia Mnara wa Mia,
ambao waliuweka wakfu hadi Mnara wa
Hananeli. 2 [c]Watu wa Yeriko wakajenga
sehemu zilizopakana nao, naye Zakuri
mwana wa Imri akajenga karibu nao.

3 [d]Lango la Samaki lilijengwa upya na
wana wa Hasenaa. Waliweka boriti zake,
na wakaweka milango yake na makomeo
na nondo. 4 [e]Meremothi mwana wa Uria,
mwana wa Hakosi, alikarabati sehemu
iliyofuatia. Baada yake Meshulamu mwana
wa Berekia, mwana wa Meshezabeli,
alifanya ukarabati na aliyemfuatia ni Sadoki
mwana wa Baana. 5 [f]Sehemu iliyofuatia
ilikarabatiwa na watu kutoka Tekoa, lakini
wakuu wao walikataa kufanya kazi chini
ya wasimamizi wao.

6 [g]Lango la Yeshana lilikarabatiwa na
Yoyada mwana wa Pasea, na Meshulamu
mwana wa Besodeya. Waliweka boriti zake,
na wakaweka milango, makomeo na nondo.
7 [h]Karibu nao ukarabati ulifanywa na watu
kutoka Gibeoni na Mispa, yaani Melati
Mgibeoni, na Yadoni Mmeronothi, sehemu
hizi zikiwa chini ya mamlaka ya mtawala
wa Ng’ambo ya Frati. 8 [i]Uzieli mwana wa
Harhaya, mmoja wa masonara, alikarabati
sehemu iliyofuatia, naye Hanania mmoja wa
watengenezaji marashi akakarabati sehemu
iliyofuatia. Walitengeneza Yerusalemu
mpaka kufikia Ukuta Mpana. 9 Refaya
mwana wa Huri, mtawala wa nusu ya
wilaya ya Yerusalemu, alikarabati sehemu
iliyofuatia. 10 Kupakana na sehemu hii,
Yedaya mwana wa Harumafu alikarabati
sehemu iliyokuwa mkabala na nyumba
yake, naye Hatushi mwana wa Hashabnea
akakarabati sehemu iliyofuatia. 11 [j]Malkiya
mwana wa Harimu, na Hashubu mwana
wa Pahath-Moabu walikarabati sehemu
nyingine pamoja na Mnara wa Matanuru.
12 [k]Shalumu mwana wa Haloheshi, mtawala
wa nusu ya wilaya ya Yerusalemu,
alikarabati sehemu iliyofuatia akisaidiwa
na binti zake.

13 [l]Lango la Bondeni lilikarabatiwa na
Hanuni na wakazi wa Zanoa. Walilijenga
upya, na kuweka milango yake na makomeo
na nondo mahali pake. Pia walikarabati
ukuta wenye urefu wa mita 450 hadi Lango
la Samadi.

14 [m]Lango la Samadi lilikarabatiwa na
Malkiya mwana wa Rekabu, mtawala wa
wilaya ya Beth-Hakeremu. Alilijenga upya,
na kuweka milango yake, na makomeo na
nondo.

15 [n]Lango la Chemchemi lilikarabatiwa na
Shalumu mwana wa Kolhoze, mtawala wa
wilaya ya Mispa. Alilijenga upya, akaliezeka
na kuweka milango yake, na makomeo na
nondo mahali pake. Pia alikarabati ukuta
wa Bwawa la Siloamu karibu na Bustani ya
Mfalme, hadi kwenye ngazi zinazoshuka
kutoka Mji wa Daudi. 16 [o]Baada yake,
Nehemia mwana wa Azbuki, mtawala wa
nusu ya wilaya ya Beth-Suri, alikarabati
kufikia mkabala na makaburi ya Daudi,
mpaka kwenye bwawa lililotengenezwa,
na kufikia Nyumba ya Mashujaa.

[a]**2:20** Ezr 4:3; Mdo 8:21; Rum 8:31
[b]**3:1** Yer 31:38; Ezr 10:24; Neh 12:39; Za 48:12; Yn 5:2; Isa 58:2; Zek 14:10
[c]**3:2** Ezr 2:34; Neh 7:36
[d]**3:3** 2Nya 33:14; Neh 12:39; Sef 1:10; Neh 6:1
[e]**3:4** Ezr 8:33
[f]**3:5** Neh 3:27; 2Sam 14:2
[g]**3:6** Neh 12:36
[h]**3:7** Yos 9:3; Neh 2:7-8
[i]**3:8** Neh 12:38
[j]**3:11** Neh 12:38; Ezr 2:32
[k]**3:12** Kut 15:25; Lk 8:3; Flp 4:3
[l]**3:13** Neh 2:13; 2Nya 26:9; Yos 15:34
[m]**3:14** Yer 6:1; Mik 1:11
[n]**3:15** Yos 18:26; Amu 20:1-3; Isa 8:6; Yn 9:7
[o]**3:16** Yos 15:58; Wim 3:7; Mdo 2:29

17 [a]Baada yake, ukarabati ulifanywa
na Walawi chini ya uongozi wa Rehumu
mwana wa Bani. Aliyefuatia ni Hashabia,
mtawala wa nusu ya wilaya ya Keila,
aliyekarabati sehemu ya wilaya yake.
18 [b]Baada yake, ukarabati ulifanywa na
ndugu zao chini ya usimamizi wa Binui
mwana wa Henadadi, mtawala wa nusu
hiyo ingine ya wilaya ya Keila. 19 [c]Baada
yao, Ezeri mwana wa Yeshua, mtawala
wa Mispa, alikarabati sehemu nyingine,
kuanzia ile sehemu inayotazamana na
mwinuko wa kuelekea kwenye ghala la
kuhifadhia silaha, mpaka kwenye pembe
ya ukuta. 20 [d]Baada yake, Baruku mwana
wa Zakai alikarabati kwa bidii sehemu
nyingine kuanzia ile pembe, mpaka kwenye
lango la nyumba ya Eliashibu kuhani mkuu.
21 [e]Kupakana naye, Meremothi mwana wa
Uria, mwana wa Hakosi, alikarabati sehemu
nyingine, kuanzia penye lango la nyumba
ya Eliashibu mpaka mwisho wake.

22 Baada yake, ukarabati ulifanywa na
makuhani waliotoka eneo lililouzunguka
mji. 23 Baada yao Benyamini na Hashubu
walikarabati mbele ya nyumba zao, na baada
yao Azaria mwana wa Maaseya, mwana
wa Anania alifanya ukarabati kando ya
nyumba yake. 24 [f]Baada yake, Binui mwana
wa Henadadi alikarabati sehemu nyingine,
kuanzia kwenye nyumba ya Azaria mpaka
kwenye pembe ya ukuta. 25 [g]Naye Palali,
mwana wa Uzai alijenga sehemu iliyokuwa
mkabala na pembe ya ukuta, mpaka
kwenye mnara wa juu ambao unajitokeza
kuanzia kwenye jumba la kifalme, kando
ya ua wa walinzi. Baada yake, Pedaya
mwana wa Paroshi, 26 [h]na watumishi wa
Hekalu walioishi juu ya kilima cha Ofeli
walikarabati hadi kufikia mkabala na Lango
la Maji, kuelekea mashariki na ule mnara
uliojitokeza. 27 [i]Baada yao, watu wa Tekoa
walikarabati sehemu nyingine, kuanzia
mnara mkubwa utokezao hadi ukuta wa
Ofeli.

28 [j]Makuhani walifanya ukarabati juu
ya Lango la Farasi, kila mmoja mbele ya
nyumba yake. 29 [k]Baada yao, Sadoki mwana
wa Imeri alifanya ukarabati mkabala na
nyumba yake. Baada yake, Shemaya mwana
wa Shekania, mlinzi wa Lango la Mashariki,
alifanya ukarabati. 30 Baada yake, Hanania
mwana wa Shelemia, na Hanuni mwana
wa sita wa Salafu walikarabati sehemu
nyingine. Baada yao, Meshulamu mwana
wa Berekia alikarabati sehemu iliyokuwa
mkabala na nyumba zake za kuishi. 31 Baada
yake Malkiya, mmoja wa masonara, alifanya
ukarabati mpaka kwenye nyumba za
watumishi wa Hekalu[l] na wafanyabiashara,
mkabala na Lango la Ukaguzi, hadi kufikia
chumba kilicho juu ya pembe. 32 [m]Masonara
na wafanyabiashara walifanya ukarabati
kutoka chumba kilichoko juu ya pembe
hadi Lango la Kondoo.

### *Upinzani Wakati Wa Ujenzi*

4 [n]Sanbalati aliposikia kwamba tulikuwa
tunajenga ukuta upya, alikasirika na
akawa na uchungu sana. Aliwadhihaki
Wayahudi 2 [o]mbele ya rafiki zake na jeshi
la Samaria, akisema, “Hawa Wayahudi
wanyonge wanafanya nini? Je, wataweza
kuurudishia ukuta wao? Je, watatoa
dhabihu? Je, wataweza kumaliza kuujenga
kwa siku moja? Je, wataweza kufufua mawe
kutoka malundo ya vifusi yaliyoungua
hivyo?”

3 [p]Tobia Mwamoni aliyekuwa upande
wake akasema, “Wanachokijenga, hata
kama mbweha angepanda juu yake, huo
ukuta wao wa mawe angeliubomoa!”

---

[a]**3:17** Yos 15:44
[b]**3:18** Yos 15:44; 1Sam 23:1
[c]**3:19** 2Nya 26:9
[d]**3:20** Mhu 9:10; Rum 12:11
[e]**3:21** Ezr 8:33
[f]**3:24** Yer 3:19; Ezr 8:33
[g]**3:25** Yer 32:2; 37:21; Ezr 2:3
[h]**3:26** Ezr 2:43; Neh 7:46; 2Nya 33:14; Neh 12:37; 8:1-3
[i]**3:27** Za 48:12; Neh 3:5
[j]**3:28** 2Nya 23:15; Yer 31:40; 2Fal 11:16
[k]**3:29** Yer 19:2
[l]31 Yaani *Wanethini*
[m]**3:32** Neh 12:39; Yn 5:2
[n]**4:1** Ezr 4:1-5; Neh 2:10
[o]**4:2** Ezr 4:9-10; Yer 26:18
[p]**4:3** Neh 2:10; Ay 13:12; 15:3

4 [a]Ee Mungu wetu, utusikie, kwa kuwa
tumedharauliwa. Warudishie matukano yao
kwenye vichwa vyao wenyewe. Uwatoe ili
wawe nyara katika nchi ya waliowateka.
5 [b]Usiusitiri uovu wao, wala usifute dhambi
zao mbele zako, kwa kuwa wamewatukana
wajenzi mbele.

6 Basi tuliujenga upya ukuta mpaka wote
ukafikia nusu ya kimo chake, kwa kuwa
watu walifanya kazi kwa moyo wote.
7 [c]Lakini wakati Sanbalati, Tobia,
Waarabu, Waamoni na watu wa Ashdodi
waliposikia kuwa ukarabati wa kuta
za Yerusalemu ulikuwa umeendelea na
mianya ilikuwa inazibwa, walikasirika
sana. 8 [d]Wote walifanya shauri pamoja
kuja kupigana dhidi ya Yerusalemu, na
kuchochea machafuko dhidi yake. 9 [e]Lakini
tulimwomba Mungu wetu, na tukaweka
ulinzi usiku na mchana kupambana na
tishio hili.
10 [f]Wakati ule ule, watu wa Yuda
wakasema, “Nguvu za wafanyakazi
zinapungua, nacho kifusi ni kingi mno, kiasi
kwamba hatuwezi kuujenga upya ukuta.”
11 Pia adui zetu walisema, “Kabla
hawajajua au kutuona, tutakuwa palepale
katikati yao, na tutawaua na kuikomesha
hiyo kazi.”
12 Kisha Wayahudi ambao waliishi
karibu nao walikuja zaidi ya mara kumi
na kutuambia, “Popote mtakapoelekea,
watatushambulia.”
13 Kwa hiyo nikaweka baadhi ya watu
nyuma ya sehemu za chini za ukuta kwenye
sehemu zilizo wazi, nikawaweka kufuatana
na jamaa zao, wakiwa na panga, mikuki
na pinde zao. 14 [g]Baada ya kuona hali
ilivyo, nikasimama na kuwaambia wakuu,
maafisa na wengine wote, “Msiwaogope.
Mkumbukeni Bwana, ambaye ni mkuu
mwenye kuogofya. Piganeni kwa ajili ya
ndugu zenu, wana wenu na binti zenu,
wake zenu na nyumba zenu.”
15 [h]Adui zetu waliposikia kwamba
tumetambua hila yao, na kwamba Mungu
amevuruga shauri lao, sote tulirudi kwenye
ukuta, kila mmoja kwenye kazi yake.
16 Kuanzia siku ile na kuendelea, nusu
ya watu wangu walifanya kazi ya ujenzi,
na nusu nyingine wakashika mikuki, ngao,
pinde na dirii. Maafisa walijipanga nyuma
ya watu wote wa Yuda 17 [i]waliokuwa
wakijenga ukuta. Wale waliobeba vifaa
vya ujenzi walifanya kazi yao kwa mkono
mmoja, na kushika silaha kwa mkono
mwingine, 18 [j]na kila mjenzi alijifunga
upanga wake upande mmoja akiwa
anafanya kazi. Lakini mtu wa kupiga
baragumu alikaa pamoja nami.
19 Kisha nikawaambia wakuu, maafisa
na watu wengine wote, “Kazi hii ni
kubwa na imeenea sehemu kubwa, nasi
tumetawanyika kila mmoja akiwa mbali
na mwenzake juu ya ukuta. 20 [k]Popote
mtakaposikia sauti ya baragumu, jiungeni
nasi huko. Mungu wetu atatupigania!”
21 Basi tuliendelea na kazi, nusu ya watu
wakishikilia mikuki, kuanzia mawio ya
jua hadi nyota zilipoonekana. 22 Wakati
huo pia niliwaambia watu, “Kila mtu na
msaidizi wake wakae ndani ya Yerusalemu
wakati wa usiku, ili waweze kutumika kama
walinzi wakati wa usiku, na kufanya kazi
wakati wa mchana.” 23 Mimi, wala ndugu
zangu, wala watu wangu, wala walinzi
waliokuwa pamoja nami hatukuvua nguo
zetu. Kila mmoja alikuwa na silaha yake,
hata alipokwenda kuchota maji.

### *Nehemia Awasaidia Maskini*

5 [l]Wakati huu wanaume na wake zao
wakalia kilio kikuu dhidi ya ndugu
zao Wayahudi. 2 [m]Baadhi yao walikuwa

[a]**4:4** Za 79:12; 123:3-4; Yer 33:24; Hos 12:14
[b]**4:5** Za 59:5-13; 2Fal 14:21; Mao 1:22; Isa 2:9; Yer 18:23
[c]**4:7** Neh 2:10
[d]**4:8** Mdo 23:12-13; Za 2:1-3; 83:1-18
[e]**4:9** Ay 22:27; Za 50:15; Mt 26:41
[f]**4:10** 1Nya 23:4
[g]**4:14** Mwa 28:15; Hes 14:9; Neh 1:5-8; Ay 37:22; 2Sam 10:12
[h]**4:15** 2Sam 17:14; Ay 5:12
[i]**4:17** 1Kor 16:13; Za 149:6
[j]**4:18** Hes 10:2
[k]**4:20** Eze 33:3; Kut 14:14; Kum 1:30; Yos 10:14
[l]**5:1** Kum 15:7; Law 25:35; Isa 5:7
[m]**5:2** Mwa 41:57; Hag 1:6

wakisema, “Sisi na wana wetu na binti zetu
tuko wengi. Ili tuweze kula na kuishi, ni
lazima tupate nafaka.”
3 [a]Wengine walikuwa wakisema,
“Tunaweka rehani mashamba yetu,
mashamba ya mizabibu, na nyumba zetu
ili tupate nafaka wakati wa njaa.”
4 [b]Bado kukawa na wengine waliokuwa
wakisema, “Ilitubidi tukope fedha ili kulipa
kodi ya mfalme kwa ajili ya mashamba yetu
na mashamba yetu ya mizabibu. 5 [c]Ingawa
sisi ni mwili na damu moja sawa na watu
wa nchi yetu, na ijapo wana wetu ni wazuri
kama wana wao, bado inatupasa kuwatoa
wana wetu na binti zetu kwenye utumwa.
Baadhi ya binti zetu wameshakuwa
watumwa tayari, lakini hatuna uwezo wa
kuwakomboa, kwa sababu mashamba yetu
na mashamba ya mizabibu yetu ni mali ya
wengine.”
6 [d]Niliposikia kilio chao na malalamiko
haya, nilikasirika sana. 7 [e]Nikayatafakari
katika akili yangu, nikiwalaumu wakuu na
maafisa. Nikawaambia, “Mnawaonea ndugu
zenu kwa kuwatoza riba!” Basi nikaitisha
mkutano mkubwa ili kuwashughulikia
8 [f]na kusema: “Kulingana na uwezo wetu,
tumewakomboa ndugu zetu Wayahudi
waliokuwa wameuzwa kwa watu
wasioamini. Sasa mnawauza ndugu zenu,
ili wauzwe tena kwetu!” Walinyamaza
kimya, kwa sababu hawakupata chochote
cha kusema.
9 [g]Basi nikaendelea kusema,
“Mnachokifanya si sawa. Je, haikuwapasa
kutembea katika hofu ya Mungu wetu
ili tuepukane na shutuma za adui zetu
wasioamini? 10 [h]Mimi na ndugu zangu
na watu wangu tunawakopesha watu
fedha na nafaka. Lakini jambo hili la
kutoza riba likome! 11 [i]Warudishieni mara
moja mashamba yao, mashamba yao ya
mizabibu, mashamba yao ya mizeituni, na
nyumba zao, pia riba yao mnayowatoza na
sehemu ya fungu la mia la fedha, nafaka,
divai mpya na mafuta.”
12 [j]Wakasema, “Tutawarudishia na
hatutataka kitu chochote zaidi kutoka
kwao. Tutafanya kama ulivyosema.”
Kisha nikawaita makuhani na kuwafanya
wakuu na maafisa kuapa kufanya kile
walichoahidi. 13 [k]Pia nikakung’uta makunjo
ya vazi langu na kusema, “Kila mtu ambaye
hatatimiza ahadi hii, Mungu na amkung’ute
hivi kutoka nyumba yake na katika mali
zake. Basi mtu wa namna hiyo akung’utiwe
nje na aachwe bila kitu!”
Waliposikia hili, mkutano wote ukasema,
“Amen,” na wakamtukuza Bwana. Nao
watu wakafanya kama walivyokuwa
wameahidi.
14 [l]Zaidi ya hayo, kutoka mwaka wa
ishirini wa Mfalme Artashasta, wakati
nilipoteuliwa kuwa mtawala wao katika nchi
ya Yuda, mpaka mwaka wake wa thelathini
na mbili, yaani miaka kumi na miwili,
mimi wala ndugu zangu hatukula chakula
ambacho kwa kawaida hupewa watawala.
15 [m]Lakini watawala wa mwanzoni, wale
walionitangulia, waliwalemea watu na
kuchukua kutoka kwao shekeli arobaini
za fedha,[n] pamoja na chakula na mvinyo.
Wasaidizi wao pia walijifanya wakuu juu
ya watu. Lakini kwa kumheshimu Mungu
sikufanya hivyo. 16 [o]Badala yake, nilijitoa
kwa bidii katika kazi ya ukuta huu. Watu
wangu wote walikutanika pale kwa ajili ya
kazi. Hatukujipatia shamba lolote.
17 Zaidi ya hayo, Wayahudi na maafisa
150 walikula mezani pangu, pamoja na
wale waliotujia kutoka mataifa jirani.

---

[a]**5:3** Mwa 47:23; Za 109:11
[b]**5:4** Ezr 4:13
[c]**5:5** Mwa 37:27; 29:14; Kum 15:7-11; 2Fal 4:1; Mt 18:25
[d]**5:6** Kut 11:8; Neh 13:8; Mk 3:5; Efe 4:26
[e]**5:7** Kut 22:25-27; Kum 24:10-13; Law 19:17
[f]**5:8** Law 25:47-48; Yer 34:8
[g]**5:9** Mwa 13:7-8; Rum 2:24; Isa 52:5; 1Pet 2:12
[h]**5:10** Kut 22:25
[i]**5:11** Isa 58:6
[j]**5:12** Ezr 10:5; Yer 34:8-9
[k]**5:13** Mt 10:14; Mdo 13:51; 18:6; Kum 27:15-26
[l]**5:14** Neh 2:6; 13:6; Mwa 42:6; 1Kor 9:4
[m]**5:15** Mwa 42:18; 20:11; Ay 31:23; Lk 18:2-4
[n]15 Shekeli 40 za fedha ni sawa na gramu 456.
[o]**5:16** 2The 3:7-10

18 [a]Kila siku niliandaliwa maksai mmoja,
kondoo sita wazuri, na kuku, na mvinyo
wa kila aina kwa wingi kila baada ya siku
kumi. Licha ya mambo haya yote, sikudai
chakula kilichokuwa fungu la mtawala, kwa
sababu madai yalikuwa mazito sana kwa
watu hawa.
19 [b]Unikumbuke kwa fadhili, Ee Mungu
wangu, kwa yote niliyofanya kwa ajili ya
watu hawa.

*Upinzani Zaidi Wakati Wa Ujenzi*

6 [c]Habari zilipofika kwa Sanbalati, Tobia,
Geshemu Mwarabu, na adui zetu wengine
kwamba nimejenga tena ukuta na hakuna
nafasi iliyobakia ndani mwake, ingawa
mpaka wakati huo sikuwa nimeweka
milango kwenye malango, 2 [d]Sanbalati na
Geshemu wakanitumia ujumbe huu: "Njoo,
tukutane katika mojawapo ya vijiji katika
nchi tambarare ya Ono."
Lakini walikuwa wakikusudia kunidhuru.
3 [e]Kwa hiyo niliwatuma wajumbe kwao
na majibu haya: "Kazi ninayoifanya ni
kubwa sana, siwezi kuja. Kwa nini niiache
kazi isimame nije kwenu?" 4 [f]Mara nne
walinitumia ujumbe wa namna iyo hiyo,
na kila mara niliwapa jibu lile lile.
5 [g]Basi, mara ya tano, Sanbalati akamtuma
msaidizi wake kwangu akiwa na ujumbe
wa aina ile ile, naye alikuwa amechukua
mkononi mwake barua isiyofungwa,
6 [h]iliyokuwa imeandikwa:

"Habari imeenezwa miongoni mwa
mataifa, naye Geshemu anasema
kwamba ni kweli, kuwa wewe na
Wayahudi mnafanya hila ya kuasi,
ndiyo sababu mnajenga ukuta. Zaidi
ya hayo, kufuatana na taarifa hizi,
karibuni utakuwa mfalme wao, 7 [i]na
hata umewateua manabii wafanye
tangazo hili kukuhusu wewe huko
Yerusalemu: 'Yuko mfalme katika
Yuda!' Sasa taarifa hii itarudishwa
kwa mfalme. Basi njoo, tufanye shauri
pamoja."

8 [j]Nilimpelekea jibu hili: "Hakuna
jambo kama hilo unalosema linalofanyika.
Unalitunga tu kwenye kichwa chako."
9 [k]Wote walikuwa wakijaribu
kutuogopesha, wakifikiri hivi: "Mikono ya
watu italegea kiasi kwamba hawataweza
kufanya kazi, nayo haitakamilika."
Lakini niliomba, "Ee Mungu, sasa nitie
mikono yangu nguvu."
10 [l]Siku moja nilikwenda nyumbani kwa
Shemaya mwana wa Delaya, mwana wa
Mehetabeli, ambaye alikuwa amefungwa
ndani ya nyumba yake. Akasema, "Tukutane
katika nyumba ya Mungu, ndani ya Hekalu,
na tufunge milango ya Hekalu, kwa sababu
watu wanakuja kukuua. Naam, wanakuja
usiku kukuua."
11 [m]Lakini nikasema, "Je, mtu kama
mimi akimbie? Au mtu kama mimi
aende Hekaluni kuokoa maisha yake?
Sitakwenda!" 12 [n]Nilitambua kwamba
Mungu hakumtuma, bali alitabiri dhidi
yangu kwa sababu Tobia na Sanbalati
walikuwa wamemwajiri. 13 [o]Alikuwa
ameajiriwa kunitisha ili kwa kufanya
jambo hili nitende dhambi, kisha waweze
kuniharibia jina langu na kuniaibisha.

14 [p]Ee Mungu wangu, wakumbuke Tobia na
Sanbalati kwa sababu ya yale waliyotenda.
Pia kumbuka nabii mke Noadia na manabii
wengine ambao wamekuwa wakijaribu
kunitisha.

*Kukamilika Kwa Ukuta*

15 Basi ukuta ukakamilika siku ya ishirini

[a]**5:18** 1Fal 4:22-23
[b]**5:19** Mwa 8:1; Neh 13:22; 2Fal 20:3
[c]**6:1** Neh 2:10-19; 3:1-3
[d]**6:2** 1Nya 8:12; Mit 26:24; Neh 11:25, 35; Za 12:2; Mit 26:24
[e]**6:3** Mit 14:15
[f]**6:4** Mit 1:10
[g]**6:5** Neh 2:10
[h]**6:6** Neh 2:19; Yer 9:3
[i]**6:7** 1Tim 5:20; Za 15:5; Mt 27:5; 15:17
[j]**6:8** Ay 13:4; Isa 59:4; Dan 11:27
[k]**6:9** Kum 33:25; Za 56:3; Isa 41:10; 2Kor 12:9
[l]**6:10** Hes 18:7
[m]**6:11** Mit 28:1
[n]**6:12** Eze 13:22-23; Neh 2:10
[o]**6:13** Yer 20:10
[p]**6:14** Neh 13:29; Kut 15:20; Yer 23:9-40; Zek 13:2-3; Ufu 2:20

na tano mwezi wa Eluli,[a] kazi ambayo
ilichukua siku hamsini na mbili. 16 [b]Adui
zetu wote waliposikia kuhusu hili, mataifa
yote yaliyotuzunguka yakaogopa na
kupoteza ujasiri, kwa sababu yalitambua
kuwa kazi hii imefanyika kwa msaada wa
Mungu wetu.
17 [c]Pia katika siku hizo wakuu wa Yuda
walikuwa wakituma barua nyingi kwa
Tobia, nayo majibu yaliyotoka kwa Tobia
yaliendelea kuwajia. 18 Kwa kuwa watu
wengi katika Yuda walikuwa wamemwapia
Tobia, kwani alikuwa mkwewe Shekania
mwana wa Ara, na Yehohanani mwanawe
alikuwa amemwoa binti wa Meshulamu
mwana wa Berekia. 19 Zaidi ya hayo,
walikuwa wakiniarifu jinsi Tobia alivyo
mtu mwema, nao walimwambia kila kitu
nilichosema. Naye Tobia alituma barua za
kunitisha.

7 [d]Baada ya ukuta kukamilika kujengwa
upya na nikaweka milango, mabawabu
wa lango, waimbaji, na Walawi waliteuliwa.
2 [e][f]Nikamweka Hanani ndugu yangu
kuwa kiongozi wa Yerusalemu, pamoja
na Hanania jemadari wa ngome, kwa
kuwa alikuwa mtu mwadilifu na mwenye
kumcha Mungu kuliko watu wengine.
3 Nikawaambia, "Malango ya Yerusalemu
yasifunguliwe mpaka jua litakapokuwa
limepanda. Walinzi wa malango wakiwa
bado kwenye zamu, waamuru wafunge
milango na waweke makomeo. Pia
wateueni wenyeji wa Yerusalemu wawe
walinzi, kila mmoja kwenye lindo lake, na
wengine karibu na nyumba zao wenyewe."

### *Orodha Ya Waliorudi Toka Uhamishoni*

**(Ezra 2:1-70)**

4 [g]Mji ulikuwa mkubwa, tena wenye nafasi
nyingi, lakini walikuwepo watu wachache
ndani yake, nazo nyumba zilikuwa bado ni
magofu. 5 [h]Hivyo Mungu wangu akaweka
moyoni mwangu kuwakusanya wakuu,
maafisa na watu wa kawaida kwa ajili ya
kuorodheshwa kulingana na jamaa zao.
Nilikuta orodha ya vizazi ya wale waliokuwa
wa kwanza kurudi toka utumwani. Haya
ndiyo niliyokuta yameandikwa humo:

6 [i]Hawa ndio watu wa jimbo
waliotoka uhamishoni, ambao
Nebukadneza mfalme wa Babeli
alikuwa amewachukua mateka
(walirudi Yerusalemu na Yuda, kila
mmoja kwenye mji wake, 7 [j]wakiwa
wamefuatana na Zerubabeli,
Yeshua, Nehemia, Azaria, Raamia,
Nahamani, Mordekai, Bilshani,
Mispereti, Bigwai, Nehumu na
Baana):

Orodha ya wanaume wa Israeli
ilikuwa:

| | |
|---|---|
| 8 [k]wazao wa Paroshi | 2,172 |
| 9 wazao wa Shefatia | 372 |
| 10 wazao wa Ara | 652 |
| 11 wazao wa Pahath-Moabu (wa jamaa ya Yeshua na Yoabu) | 2,818 |
| 12 wazao wa Elamu | 1,254 |
| 13 wazao wa Zatu | 845 |
| 14 wazao wa Zakai | 760 |
| 15 wazao wa Binui | 648 |
| 16 wazao wa Bebai | 628 |
| 17 wazao wa Azgadi | 2,322 |
| 18 wazao wa Adonikamu | 667 |
| 19 wazao wa Bigwai | 2,067 |
| 20 [l]wazao wa Adini | 655 |
| 21 wazao wa Ateri (kupitia Hezekia) | 98 |
| 22 wazao wa Hashumu | 328 |
| 23 wazao wa Besai | 324 |
| 24 wazao wa Harifu | 112 |
| 25 wazao wa Gibeoni | 95 |
| 26 [m]watu wa Bethlehemu na Netofa | 188 |

[a]15 Eluli ni mwezi wa sita kwenye kalenda ya Kiyunani; katika kalenda yetu ni Agosti/Septemba.
[b]**6:16** Neh 2:10; 4:1; 6:1; Za 126:2
[c]**6:17** 2Sam 9:7; 1Fal 18:19
[d]**7:1** 1Nya 26:12-19; Neh 6:1; 8:9; Za 68:25
[e]**7:2** Neh 10:23; 2:8; Mit 26:24; 1Fal 18:3
[f]**7:2** Neh 7:3
[g]**7:4** Mit 1:10; Neh 11:1
[h]**7:5** Mit 2:6; Rum 11:36; 1Kor 4:7; 2Kor 8:16; Yak 1:17; Ezr 2:1-70
[i]**7:6** Ezr 2:1-10; 2Nya 36:20
[j]**7:7** 1Nya 3:19; Ezr 2:2
[k]**7:8** Ay 13:4; Dan 11:27
[l]**7:20** Ezr 8:6
[m]**7:26** 2Sam 23:28; Mwa 35:6; Rut 2; 4

27 [a]watu wa Anathothi 128
28 watu wa Beth-Azmawethi 42
29 [b]watu wa Kiriath-Yearimu, Kefira na Beerothi 743
30 watu wa Rama na Geba 621
31 [c]watu wa Mikmashi 122
32 [d]watu wa Betheli na Ai 123
33 watu wa Nebo 52
34 wazao wa Elamu 1,254
35 wazao wa Harimu 320
36 [e]wazao wa Yeriko 345
37 [f]wazao wa Lodi, Hadidi na Ono 721
38 wazao wa Senaa 3,930

39 [g]Makuhani:
wazao wa Yedaya (kwa jamaa ya Yeshua) 973
40 [h]wazao wa Imeri 1,052
41 [i]wazao wa Pashuri 1,247
42 [j]wazao wa Harimu 1,017

43 Walawi:
wazao wa Yeshua (kupitia Kadmieli kupitia jamaa ya Hodavia) 74

44 [k]Waimbaji:
wazao wa Asafu 148

45 [l]Mabawabu wa malango:
wazao wa Shalumu, Ateri, Talmoni, Akubu, Hatita na Shobai 138

46 [m]Watumishi wa Hekalu:[n]
wazao wa Siha, Hasufa, Tabaothi,
47 wazao wa Kerosi, Sia, Padoni,
48 wazao wa Lebana, Hagaba, Shalmai,
49 wazao wa Hanani, Gideli, Gahari,
50 wazao wa Reaya, Resini, Nekoda,
51 wazao wa Gazamu, Uza, Pasea,
52 wazao wa Besai, Meunimu, Nefusimu,
53 wazao wa Bakbuki, Hakufa, Harhuri,
54 wazao wa Basluthi, Mehida, Harsha,
55 wazao wa Barkosi, Sisera, Tema,
56 wazao wa Nesia na Hatifa.

57 [o]Wazao wa watumishi wa Solomoni:
wazao wa Sotai, Soferethi, Perida,
58 wazao wa Yaala, Darkoni, Gideli,
59 wazao wa Shefatia, Hatili, Pokereth-Hasebaimu na Amoni.
60 [p]Watumishi wa Hekalu wote na wazao wa watumishi wa Solomoni 392

61 [q]Wafuatao walikuja kutoka miji ya Tel-Mela, Tel-Harsha, Kerubu, Adoni na Imeri, lakini hawakuweza kuthibitisha kwamba jamaa zao zilikuwa uzao wa Israeli:
62 wazao wa Delaya, Tobia na Nekoda 642

63 [r]Na kutoka miongoni mwa makuhani:
wazao wa Hobaya, Hakosi na Barzilai (mtu aliyekuwa amemwoa binti wa Barzilai, Mgileadi, naye akaitwa kwa jina hilo).
64 Hawa walitafuta orodha za jamaa
zao, lakini hawakuonekana humo,
kwa hiyo waliondolewa kutoka
kundi la makuhani, kwa kuwa
walihesabiwa kuwa najisi. 65 [s]Kwa
hiyo, mtawala[t] aliagiza kuwa
wasile chochote miongoni mwa
vyakula vitakatifu hadi kuwe kuhani

[a]**7:27** Yos 21:18; Ezr 2:23
[b]**7:29** Yos 18:25-26
[c]**7:31** 1Sam 13:2; Isa 10:27
[d]**7:32** Mwa 12:8
[e]**7:36** Neh 3:2
[f]**7:37** 1Nya 8:12
[g]**7:39** 1Nya 24:7
[h]**7:40** 1Nya 24:14
[i]**7:41** 1Nya 9:12; 24:9
[j]**7:42** 1Nya 24:8; Ezr 10:31
[k]**7:44** Neh 11:23
[l]**7:45** 1Nya 9:17
[m]**7:46** Neh 3:26
[n]46 Yaani *Wanethini*
[o]**7:57** Mwa 9:25, 26; 1Fal 5:13, 14; 2Nya 2:17, 18
[p]**7:60** 1Nya 9:2
[q]**7:61** Ezr 2:59
[r]**7:63** 2Sam 17:27; 19:31-34; 1Fal 2:7; Ezr 2:61
[s]**7:65** Kut 28:30; Neh 8:9; Hes 7:89; 27:18-21
[t]65 Au *Tirshatha*

atakayehudumu kwa Urimu na
Thumimu.[a]

66 Jumla ya watu wote waliorudi
walikuwa 42,360; 67 tena zaidi
ya hao walikuwepo watumishi
wa kiume na wa kike 7,337; pia
walikuwamo waimbaji wanaume
na wanawake 245. 68 Walikuwa na
farasi 736, nyumbu 245 69 ngamia
435 na punda 6,720.

70 [b]Baadhi ya viongozi wa jamaa
walichangia kazi ya ujenzi. Mtawala
alikabidhi kwenye hazina darkoni
1,000[c] za dhahabu, mabakuli 50, na
mavazi 530 kwa ajili ya makuhani.
71 [d]Baadhi ya viongozi wa jamaa
walikabidhi kwenye hazina darkoni
20,000 za dhahabu,[e] na mane 2,200[f]
za fedha kwa ajili ya kazi hiyo.
72 [g]Jumla ya matoleo ya watu
wengine yalikuwa ni darkoni 20,000
za dhahabu, mane 2,000 za fedha, na
mavazi sitini na saba ya makuhani.
73 [h]Makuhani, Walawi, mabawabu,
waimbaji na watumishi wa Hekalu,
pamoja na baadhi ya watu wengine
na Waisraeli waliosalia waliishi katika
miji yao wenyewe.

*Ezra Asoma Sheria*

Ilipotimia miezi saba, nao Waisraeli
wakiwa tayari wanaishi katika miji yao,
8 [i]watu wote wakakusanyika kama mtu
mmoja kwenye uwanja mbele ya Lango
la Maji. Wakamwambia Ezra mwandishi
alete Kitabu cha Sheria ya Mose, ambacho
BWANA aliamuru kwa ajili ya Israeli.
2 [j]Basi katika siku ya kwanza ya mwezi
wa saba, kuhani Ezra akaleta Sheria mbele
ya kusanyiko, ambamo walikuwamo
wanaume, wanawake na watu wote
walioweza kufahamu. 3 [k]Akaisoma kwa
sauti kubwa tangu mapambazuko mpaka
adhuhuri, akiwa ameuelekea uwanja
uliokuwa mbele ya Lango la Maji mbele
ya wanaume, wanawake na wengine
ambao waliweza kufahamu. Watu wote
wakasikiliza kwa makini kile Kitabu cha
Sheria.
4 [l]Mwandishi Ezra alikuwa amesimama
juu ya jukwaa la miti lililojengwa kwa
kusudi hilo. Karibu naye upande wa kuume
alisimama Matithia, Shema, Anaya, Uria,
Hilkia na Maaseya. Upande wake wa
kushoto walikuwepo Pedaya, Mishaeli,
Malkiya, Hashumu, Hashbadani, Zekaria
na Meshulamu.
5 [m]Ezra akakifungua kile kitabu. Watu
wote waliweza kumwona kwa sababu
alikuwa amesimama juu zaidi, naye
alipokifungua watu wote wakasimama.
6 [n]Ezra akamsifu BWANA, Mungu mkuu,
nao watu wote wakainua mikono yao na
kuitikia, "Amen! Amen!" Kisha wakasujudu
na kumwabudu BWANA hali nyuso zao
zikigusa ardhi.
7 [o]Watu wakiwa wamesimama pale,
Walawi wafuatao waliwafunza ile Sheria:
Yeshua, Bani, Sherebia, Yamini, Akubu,
Shabethai, Hodia, Maaseya, Kelita, Azaria,
Yozabadi, Hanani na Pelaya. 8 [p]Walisoma
kutoka kile Kitabu cha Sheria ya Mungu,

---

[a]65 Urimu na Thumimu maana yake ni Nuru na Kweli; vifaa hivi viliwekwa kwenye kifuko cha juu cha kisibau cha kuhani mkuu ili kujua mapenzi ya Mungu kwenye mambo ya kutatanisha.
[b]**7:70** Neh 8:9; 10:1
[c]70 Darkoni 1,000 za dhahabu ni sawa na uzito wa kilo 8.6.
[d]**7:71** 1Nya 29:7; Ezr 2:69
[e]71 Darkoni 20,000 za dhahabu ni sawa na kilo 172.
[f]71 Mane 2,200 za fedha ni sawa na kilo 1,300.
[g]**7:72** Ay 34:10; Kut 25:2
[h]**7:73** Za 34:20; Neh 11:20; Kut 23:14-17; Law 23:24-44; Ezr 3:1
[i]**8:1** Neh 3:28; Ezr 7:6; 2Nya 34:15; Neh 3:26; Kum 28:61; 2Nya 34:15
[j]**8:2** Law 23:23-25; Hes 29:1-6; Kum 31:11
[k]**8:3** Neh 3:26
[l]**8:4** 2Nya 6:13
[m]**8:5** Amu 3:20
[n]**8:6** Kut 4:31; Hes 5:22; Neh 5:13; 1Tim 2:8; Ezr 9:5; 1Tim 2:8
[o]**8:7** Ezr 10:23; Law 10:11; 2Nya 17:1
[p]**8:8** Hab 2:2; Mdo 8:30-35

wakiifafanua na kuwapa maelezo ili
watu waweze kufahamu kile kilichokuwa
kikisomwa.
9 [a]Ndipo Nehemia aliyekuwa mtawala,[b]
Ezra kuhani na mwandishi, pamoja na
Walawi waliokuwa wakiwafundisha watu
wakawaambia wote, "Siku hii ni takatifu
kwa Bwana Mungu wenu. Msiomboleze
wala msilie." Kwa kuwa watu wote
walikuwa wakilia walipokuwa wakisikiliza
maneno ya ile Sheria.
10 [c]Nehemia akasema, "Nendeni
mkafurahie chakula kizuri na vinywaji
vitamu, na mpeleke sehemu kwa wale
ambao hawana chochote cha kula. Siku hii
ni takatifu kwa Bwana. Msihuzunike, kwa
kuwa furaha ya Bwana ni nguvu zenu."
11 Walawi wakawatuliza watu wote
wakisema, "Kuweni watulivu, kwa kuwa
hii ni siku takatifu. Msihuzunike."
12 [d]Kisha watu wote wakaondoka kwenda
kula na kunywa, na kupeana sehemu ya
chakula, na wakaadhimisha kwa furaha
kubwa, kwa sababu sasa walifahamu
maneno yale waliyokuwa wameelezwa.
13 Katika siku ya pili ya mwezi, wakuu
wa mbari zote, pamoja na makuhani na
Walawi, walikusanyika wakimzunguka
Ezra mwandishi ili wapate kusikiliza kwa
makini maneno ya Sheria. 14 [e]Wakakuta
imeandikwa katika ile Sheria, ambayo
Bwana aliiamuru kupitia kwa Mose,
kwamba Waisraeli walipaswa kukaa katika
vibanda wakati wa sikukuu ya mwezi wa
saba, 15 [f]na kwamba walipaswa kutangaza
neno hili na kulieneza katika miji yao na
katika Yerusalemu wakisema: "Enendeni
katika nchi ya mlima na kuleta matawi
kutoka miti ya mizeituni, mizeituni mwitu,
mihadasi, mitende na miti ya kivuli, ili
kutengeneza vibanda," kama ilivyoandikwa.
16 [g]Basi watu wakaenda na kuleta matawi,
nao wakajijengea vibanda juu ya paa za
nyumba zao, katika nyua zao, katika nyua
za nyumba ya Mungu, na katika uwanja
karibu na Lango la Maji na uwanja wa
Lango la Efraimu. 17 [h]Jamii yote ya watu
waliorudi kutoka utumwani wakajenga
vibanda na kuishi ndani yake. Tangu wakati
wa Yoshua mwana wa Nuni mpaka siku
ile, Waisraeli hawakuwahi kuiadhimisha
namna hii. Furaha yao ilikuwa kubwa sana.
18 [i]Siku baada ya siku, kuanzia siku ya
kwanza hadi ya mwisho, Ezra alisoma
kutoka kwenye kile Kitabu cha Sheria ya
Mungu. Wakaiadhimisha sikukuu ile kwa
siku saba, nayo siku ya nane, kufuatana na
maagizo, kulikuwa na kusanyiko maalum.

*Waisraeli Waungama Dhambi Zao*

9 [j]Katika siku ya ishirini na nne ya mwezi
ule ule, Waisraeli walikusanyika pamoja,
wakifunga na kuvaa nguo za gunia na
kujitia mavumbi vichwani mwao. 2 [k]Wale
wa uzao wa Israeli walijitenga na wageni
wote. Wakasimama mahali pao, na
kuungama dhambi zao na uovu wa baba
zao. 3 [l]Wakasimama pale walipokuwa,
wakasoma kutoka kwenye kile Kitabu cha
Sheria ya Bwana Mungu wao kwa muda
wa robo siku, na wakatumia robo nyingine
kwa kuungama dhambi na kumwabudu
Bwana Mungu wao. 4 [m]Walawi wafuatao
walikuwa wamesimama kwenye ngazi:
Yeshua, Bani, Kadmieli, Shebania, Buni,
Sherebia, Bani na Kenani. Hawa walimlilia
Bwana Mungu wao kwa sauti kubwa.
5 [n]Nao Walawi Yeshua, Kadmieli, Bani,
Hashabnea, Sherebia, Hodia, Shebania na
Pethahia wakasema: "Simameni mkamsifu
Bwana Mungu wenu, yeye ambaye ni
Mungu tangu milele hata milele.

"Libarikiwe jina lake tukufu,

[a]**8:9** Ezr 2:63; Neh 7:65; Kum 12:7-12; 16:14-15
[b]9 Au *Tirshatha*
[c]**8:10** Es 9:22; Lk 14:12-14; Law 23:40; Kum 12:18
[d]**8:12** Es 9:22
[e]**8:14** Mwa 33:17; Law 23:34
[f]**8:15** Law 23:4; Kum 16:16; Law 23:40
[g]**8:16** Kum 22:3; 2Fal 14:13; 2Nya 25:23
[h]**8:17** 1Fal 8:2; 2Nya 7:8
[i]**8:18** Kum 33:10; Hes 29:35; Law 23:36
[j]**9:1** Law 26:40-45; Yos 7:6; 1Sam 4:12
[k]**9:2** Ezr 6:21; Neh 13:3
[l]**9:3** Neh 8:7
[m]**9:4** Ezr 10:23
[n]**9:5** Za 78:4; Kut 15:6-11; 1Nya 29:13

litukuzwe juu ya baraka zote na sifa.
6 [a]Wewe peke yako ndiwe Bwana.
Uliziumba mbingu, hata mbingu za
mbingu na jeshi lote la mbinguni,
dunia na vyote vilivyo ndani yake, na
pia bahari na vyote vilivyomo ndani
yake. Huvipa vitu vyote uhai, nalo
jeshi la mbinguni linakuabudu wewe.
7 [b]“Wewe ni Bwana Mungu
uliyemchagua Abramu na kumtoa
kutoka Uru ya Wakaldayo, nawe
ukamwita Abrahamu. 8 [c]Uliona kuwa
moyo wake ni mwaminifu kwako,
nawe ukafanya Agano naye kuwapa
wazao wake nchi ya Wakanaani,
Wahiti, Waamori, Waperizi, Wayebusi
na Wagirgashi. Umetimiza ahadi yako
kwa sababu wewe ni mwenye haki.
9 [d]“Uliona mateso ya baba zetu huko
Misri, ukasikia kilio chao huko Bahari
ya Shamu. 10 [e]Ulituma ishara za miujiza
na maajabu dhidi ya Farao, dhidi ya
maafisa wake wote na watu wote wa
nchi yake, kwa kuwa ulifahamu jinsi
Wamisri walivyowafanyia ufidhuli.
Ukajifanyia jina linalodumu hadi
leo. 11 [f]Ukagawa bahari mbele yao, ili
waweze kupita katikati yake penye
nchi kavu, lakini uliwatupa Wamisri
waliowafuatilia katika vilindi, kama
jiwe kwenye maji mengi. 12 [g]Mchana
uliwaongoza kwa nguzo ya wingu, na
usiku kwa nguzo ya moto kuwamulikia
njia iliyowapasa kuiendea.
13 [h]“Ulishuka katika Mlima Sinai,
ukanena nao kutoka mbinguni.
Uliwapa masharti na sheria zile
ambazo ni za kweli na haki, pia amri
na maagizo mazuri. 14 [i]Uliwafahamisha
Sabato yako takatifu na ukawapa amri,
maagizo na sheria kupitia mtumishi
wako Mose. 15 [j]Katika njaa yao uliwapa
mkate kutoka mbinguni, na katika kiu
yao uliwatolea maji kutoka kwenye
mwamba. Uliwaambia waingie na
kuimiliki nchi ambayo ulikuwa umeapa
kuwapa kwa mkono ulioinuliwa.
16 [k]“Lakini wao, baba zetu, wakawa
na kiburi na shingo ngumu, nao
hawakutii maagizo yako. 17 [l]Wakakataa
kusikiliza na kushindwa kukumbuka
miujiza uliyoifanya miongoni mwao.
Wakawa na shingo ngumu, na katika
uasi wao wakamchagua kiongozi ili
warudi kwenye utumwa wao. Lakini
wewe ni Mungu mwenye kusamehe,
mwenye neema na mwingi wa huruma,
si mwepesi wa hasira, ni mwingi wa
upendo. Kwa hiyo hukuwaacha, 18 [m]hata
wakati walijitengenezea sanamu ya
ndama ya kusubu na kusema, ‘Huyu
ni mungu wenu, aliyewapandisha
kutoka nchi ya Misri,’ au walipofanya
makufuru makubwa.
19 [n]“Kwa sababu ya huruma zako
kuu hukuwaacha jangwani. Wakati wa
mchana ile nguzo ya wingu haikukoma
kuwaongoza katika njia yao, wala nguzo
ya moto haikuacha kuwamulikia usiku
njia iliyowapasa kuiendea. 20 [o]Uliwapa
Roho wako mwema ili kuwafundisha.
Hukuwanyima mana yako vinywani
mwao, nawe ukawapa maji kwa ajili
ya kiu yao. 21 [p]Kwa miaka arobaini
uliwatunza jangwani. Hawakukosa
chochote, na nguo zao hazikuchakaa
wala miguu yao haikuvimba.
22 [q]“Uliwapa falme na mataifa,

[a]**9:6** Kum 6:4; Isa 37:16; Kut 8:19; Mk 12:29; Mdo 4:24
[b]**9:7** Mwa 11:28-31; 17:5
[c]**9:8** Ezr 9:1; Yos 23:14; 21:45; Mwa 15:6; Ezr 9:15
[d]**9:9** Kut 2:23-25; 14:10-30
[e]**9:10** Za 74:9; Kut 9:16; Yer 32:20; Dan 9:15
[f]**9:11** Kut 14:21; 15:4-5; Za 78:13; Ebr 11:29
[g]**9:12** Kut 13:21; 15:13
[h]**9:13** Kut 19:11, 19; Za 119:137; Kum 4:7-8; Rum 7:12
[i]**9:14** Mwa 2:3; Kut 20:8-11
[j]**9:15** Za 78:24-25; Yn 6:31; Kut 16:14-15; Hes 20:7-13
[k]**9:16** Kum 1:26-33; 31:27-29; Yer 19:15
[l]**9:17** Kut 34:6; Amu 8:34; Kut 22:27; Hes 14:1-4; Eze 5:6
[m]**9:18** Kut 32:4
[n]**9:19** Za 106:45; Kut 13:21, 22; Hes 14:14
[o]**9:20** Hes 9:17; Hag 2:5; Kut 16:15; 17:6
[p]**9:21** Kum 2:7; 8:4
[q]**9:22** Hes 21:21, 33; Kum 2:26–3:11; Mwa 15:5

ukiwagawia hata mipaka ya mbali.
Wakaimiliki nchi ya Sihoni mfalme
wa Heshboni, na nchi ya Ogu mfalme
wa Bashani. 23 [a]Uliwafanya wana wao
kuwa wengi kama nyota za angani,
nawe ukawaleta katika nchi ambayo
uliwaambia baba zao kuingia na
kuimiliki. 24 [b]Wana wao wakaingia na
kuimiliki nchi. Uliwatiisha Wakanaani
mbele yao, walioishi katika nchi,
ukawatia Wakanaani mikononi mwao,
pamoja na wafalme wao na watu wa
nchi, wawafanyie kama wapendavyo.
25 [c]Wakateka miji yenye ngome na nchi
yenye rutuba, wakamiliki nyumba
zilizojazwa na vitu vizuri vya kila
aina, visima vilivyochimbwa tayari,
mashamba ya mizabibu, mashamba
ya mizeituni na miti yenye matunda
kwa wingi. Wakala, wakashiba nao
wakanawiri sana, wakajifurahisha
katika wema wako mwingi.

26 [d]"Lakini hawakukutii nao wakaasi
dhidi yako, wakatupa sheria zako
nyuma yao. Wakawaua manabii
wako, waliowaonya ili wakurudie,
na wakafanya makufuru makubwa.
27 [e]Hivyo ukawatia mikononi mwa
adui zao, ambao waliwatesa. Lakini
walipoteswa, wakakulilia wewe.
Kutoka mbinguni uliwasikia, nawe kwa
huruma zako kuu ukawapa waokozi,
waliowaokoa kutoka mikononi mwa
adui zao.

28 [f]"Lakini mara walipokuwa na
raha, wakafanya maovu tena machoni
pako. Kisha ukawaacha mikononi
mwa adui zao, nao wakawatawala.
Walipokulilia tena, ukasikia kutoka
mbinguni, na kwa huruma zako
ukawaokoa kila mara.

29 [g]"Ukawaonya warudi katika
sheria yako, lakini wakawa na kiburi
na hawakutii amri zako. Wakatenda
dhambi dhidi ya maagizo yako
ambayo kwayo mtu ataishi kama
akiyatii. Kwa ukaidi wakakugeuzia
kisogo, wakawa na shingo ngumu na
wakakataa kusikiliza. 30 [h]Kwa miaka
mingi ulikuwa mvumilivu kwao. Kwa
njia ya Roho wako ukawaonya kupitia
manabii wako. Hata hivyo hawakujali,
basi ukawatia mikononi mwa mataifa
jirani. 31 [i]Lakini kwa rehema zako kuu
hukuwakomesha wala kuwaacha, kwa
kuwa wewe ni Mungu mwenye neema
na rehema.

32 [j]"Basi sasa, Ee Mungu wetu, uliye
mkuu, mwenye nguvu na Mungu wa
kuogofya, mwenye kushika agano
lake la upendo, usiache taabu hizi
zote zionekane kuwa kitu kidogo
mbele za macho yako, taabu hizi
zilizotupata, juu ya wafalme wetu na
viongozi, juu ya makuhani wetu na
manabii, juu ya baba zetu na watu
wako wote, tangu siku za wafalme wa
Ashuru hadi leo. 33 [k]Katika hayo yote
yaliyotupata, umekuwa mwenye haki,
na umetenda kwa uaminifu, wakati
sisi tumetenda mabaya. 34 [l]Wafalme
wetu, viongozi wetu, makuhani wetu
na baba zetu hawakufuata sheria
yako. Hawakuzingatia amri zako
wala maonyo uliyowapa. 35 [m]Hata
walipokuwa wangali katika ufalme
wao, wakiufurahia wema wako mkuu
katika nchi kubwa na yenye rutuba
uliyowapa, hawakukutumikia wala
kugeuka kutoka njia zao mbaya.

36 [n]"Lakini tazama, sisi ni watumwa
leo, watumwa katika nchi uliyowapa

[a]**9:23** Mwa 12:2; Law 26:9; Hes 10:36
[b]**9:24** Yos 11:23; Amu 4:23; 2Nya 14:13
[c]**9:25** Kum 6:10-12; Hes 13:27; Kum 8:8-11; Eze 20:6
[d]**9:26** Mdo 7:52
[e]**9:27** Hes 25:17; Za 51:1
[f]**9:28** Kut 32:22; Amu 2:17; 2Sam 24:14; Za 22:4; 106:43; 136:24
[g]**9:29** Za 5:5; Kum 4:29; Isa 2:11; Kum 30:16; Yer 25:3-7; Zek 7:11-12
[h]**9:30** Isa 63:10; 1Fal 17:13-18; 2Nya 36:16
[i]**9:31** Yer 5:10; 4:27; Isa 48:9
[j]**9:32** 2Fal 17:3; 1Fal 8:23; Ay 9:19
[k]**9:33** Mwa 18:25; Dan 9:14
[l]**9:34** 2Fal 23:11; Yer 44:17
[m]**9:35** Isa 63:7; Kum 28:45-48
[n]**9:36** Kum 28:48; Ezr 9:9

baba zetu ili wapate kula matunda yake
na vitu vingine vizuri inayozalisha.
37 [a]Kwa sababu ya dhambi zetu, mavuno
yake mengi huenda kwa wafalme
uliowaweka watutawale. Wanatawala
juu ya miili yetu na mifugo yetu kama
wapendavyo. Tuko katika dhiki kuu.

*Mapatano Ya Watu*

38 [b]"Kwa sababu ya haya yote, tunajifunga
katika mapatano, na kuyaandika, nao
viongozi wetu, Walawi wetu na makuhani
wetu wanatia mihuri yao."

10 [c]Wale waliotia muhuri walikuwa:

Nehemia mtawala,
mwana wa Hakalia.

Sedekia, 2 [d]Seraya, Azaria, Yeremia,
3 [e]Pashuri, Amaria, Malkiya,
4 Hatushi, Shebania, Maluki,
5 [f]Harimu, Meremothi, Obadia,
6 Danieli, Ginethoni, Baruku,
7 Meshulamu, Abiya, Miyamini,
8 [g]Maazia, Bilgai na Shemaya.
Hawa ndio waliokuwa makuhani.

9 [h]Walawi:

Yeshua mwana wa Azania, Binui wa
wana wa Henadadi, Kadmieli,
10 na wenzao: Shebania,
Hodia, Kelita, Pelaya, Hanani,
11 Mika, Rehobu, Hashabia,
12 Zakuri, Sherebia, Shebania,
13 Hodia, Bani na Beninu.

14 Viongozi wa watu:

Paroshi, Pahath-Moabu, Elamu, Zatu,
Bani,
15 Buni, Azgadi, Bebai,
16 [i]Adoniya, Bigwai, Adini,
17 Ateri, Hezekia, Azuri,
18 Hodia, Hashumu, Besai,
19 Harifu, Anathothi, Nebai,
20 [j]Magpiashi, Meshulamu, Heziri,
21 Meshezabeli, Sadoki, Yadua,
22 Pelatia, Hanani, Anaya,
23 Hoshea, Hanania, Hashubu,
24 Haloheshi, Pilha, Shobeki,
25 Rehumu, Hashabna, Maaseya,
26 Ahiya, Hanani, Anani,
27 Maluki, Harimu na Baana.

28 [k]"Watu wengine wote, wakiwa
ni makuhani, Walawi, mabawabu,
waimbaji, watumishi wa Hekalu,[l] na
wale wote waliojitenga na mataifa
jirani kwa ajili ya Sheria ya Mungu,
pamoja na wake zao na wana wao na
binti zao wote waliokuwa na uwezo
wa kufahamu, 29 [m]basi hawa wote
wanajiunga na ndugu zao na wakuu
wao, na kujifunga kwa laana na
kwa kiapo kufuata Sheria ya Mungu
iliyotolewa kupitia kwa Mose mtumishi
wa Mungu, na kutii kwa uangalifu amri
zote, maagizo na sheria za BWANA,
Bwana wetu.
30 [n]"Tunaahidi kutowaoza binti zetu
kwa watu wanaotuzunguka, wala
kuwaoza wana wetu binti zao.
31 [o]"Wakati mataifa jirani waletapo
bidhaa zao au nafaka kuuza siku ya
Sabato, hatutazinunua kutoka kwao
siku ya Sabato, wala siku nyingine
yoyote takatifu. Kila mwaka wa saba,
tutaacha kuilima ardhi na tutafuta
madeni yote.
32 [p]"Tunakubali wajibu wa kutimiza
amri za kutoa theluthi ya shekeli[q]
kila mwaka kwa ajili ya utumishi
wa nyumba ya Mungu: 33 [r]Kwa ajili

[a]**9:37** Kum 28:33; Mao 5:5
[b]**9:38** 2Nya 23:16; Isa 44:5
[c]**10:1** Neh 8:9; 1:1
[d]**10:2** Ezr 2:2
[e]**10:3** 1Nya 9:12
[f]**10:5** 1Nya 24:8
[g]**10:8** Neh 12:1
[h]**10:9** Neh 12:8
[i]**10:16** Ezr 8:6
[j]**10:20** 1Nya 24:15
[k]**10:28** Za 135:1; 1Nya 6:26; Neh 9:2; 13:3
[l]28 Yaani *Wanethini*
[m]**10:29** Hes 5:21; Neh 5:12; Kum 29:12
[n]**10:30** Kut 34:16; Kum 7:3; Mwa 6:2
[o]**10:31** Eze 23:38; Amo 8:5; Neh 8:5; 13:15; Kut 23:11; Kum 15:1; Law 25:1-7
[p]**10:32** Mwa 28:22
[q]32 Theluthi ya shekeli hapa kama gramu 4.
[r]**10:33** Law 24:5-6; Hes 10:10; Za 81:3; 2Nya 24:5

ya mikate ya Wonyesho, kwa ajili ya sadaka za kawaida za nafaka na sadaka za kuteketezwa, kwa ajili ya sadaka za siku za Sabato, Sikukuu za Mwandamo wa Mwezi na sikukuu nyingine zilizoamriwa, kwa ajili ya sadaka takatifu, kwa ajili ya sadaka za dhambi ili kufanya upatanisho kwa ajili ya Israeli, na kwa ajili ya kazi zote za nyumba ya Mungu wetu.

34 [a]"Sisi makuhani, Walawi na watu, tumepiga kura kuamua kuwa kila mmoja wa jamaa zetu lazima alete katika nyumba ya Mungu wetu kwa nyakati maalum kila mwaka mchango wa kuni za kukokea moto katika madhabahu ya BWANA Mungu wetu, kama ilivyoandikwa katika Sheria.

35 [b]"Pia tunachukua wajibu wa kuleta malimbuko ya mazao yetu na matunda ya kwanza ya kila mti wa matunda katika nyumba ya BWANA kila mwaka.

36 [c]"Kama pia ilivyoandikwa katika Sheria, tutawaleta wazaliwa wetu wa kwanza wa kiume, na wa mifugo yetu, yaani wa ng'ombe wetu na wa makundi yetu ya kondoo na mbuzi, katika nyumba ya Mungu wetu, kwa ajili ya makuhani wanaohudumu huko.

37 [d]"Zaidi ya hayo, tutaleta katika ghala za nyumba ya Mungu wetu, kwa makuhani, vyakula vya kwanza vya mashamba yetu, sadaka zetu za nafaka, matunda ya miti yetu yote, divai yetu mpya na mafuta. Nasi tutaleta zaka za mazao yetu kwa Walawi, kwa kuwa Walawi ndio ambao hukusanya zaka katika miji yote tunakofanya
kazi. 38 [e]Kuhani atokanaye na uzao wa Aroni atashirikiana na Walawi wakati wanapopokea zaka, nao Walawi itawapasa kuleta sehemu ya kumi ya zaka katika nyumba ya Mungu wetu katika ghala za hazina.
39 [f]Watu wa Israeli pamoja na Walawi itawapasa kuleta michango yao ya nafaka, divai mpya na mafuta katika vyumba vya ghala, mahali vifaa vya mahali patakatifu vinapohifadhiwa, na wanapokaa makuhani wanaohudumu, na mabawabu na waimbaji.

"Hatutaacha kuijali nyumba ya Mungu wetu."

*Wakazi Wapya Wa Yerusalemu*

11 [g]Basi viongozi wa watu walikaa Yerusalemu, nao watu wale wengine walipiga kura ili kuleta mtu mmoja kati ya watu kumi aje kuishi Yerusalemu, mji mtakatifu, nao wengine tisa waliobaki
wakae katika miji yao wenyewe. 2 [h]Watu waliwasifu wale wote waliojitolea kuishi Yerusalemu.

3 [i]Hawa ndio viongozi wa majimbo waliokuja kuishi Yerusalemu (baadhi ya Waisraeli, makuhani, Walawi, watumishi wa Hekalu,[j] na wazao wa watumishi wa Solomoni waliendelea kuishi katika miji ya Yuda, kila mmoja katika milki yake mwenyewe katika miji mbalimbali,
4 [k]ambapo watu wengine kutoka Yuda na Benyamini waliishi Yerusalemu).

Kutoka wazao wa Yuda:

Athaya mwana wa Uzia, mwana wa Zekaria, mwana wa Amaria, mwana wa Shefatia, mwana wa Mahalaleli, mzao
wa Peresi. 5 Naye Maaseya mwana wa Baruku, mwana wa Kolhoze, mwana wa Hazaya, mwana wa Adaya, mwana wa Yoyaribu, mwana wa Zekaria,
mzao wa Mshiloni. 6 Wazao wa Peresi walioishi Yerusalemu walikuwa 468, watu wenye uwezo.

7 Kutoka wazao wa Benyamini:

Salu mwana wa Meshulamu, mwana

[a]**10:34** Neh 13:31; Law 6:12; 16:8
[b]**10:35** Kut 23:19; Hes 18:12; Kum 26:2
[c]**10:36** Kut 13:2-12; Hes 18:14-16; Law 27:26-27
[d]**10:37** Law 23:17; Hes 15:19; Law 27:30; Hes 18:21; Kum 14:22-29
[e]**10:38** Hes 18:26; 2Nya 31:11
[f]**10:39** Neh 13:10-12; Kum 12:6; Mt 18:20
[g]**11:1** Isa 48:2; Neh 7:4; Isa 64:10; Zek 14:20-21
[h]**11:2** Amu 5:9
[i]**11:3** 1Nya 9:29; Ezr 2:44-45
[j]3 Yaani *Wanethini*
[k]**11:4** Ezr 1:5; Mwa 38:29; Ezr 2:70; 1Nya 9:3

wa Yoedi, mwana wa Pedaya, mwana
wa Kolaya, mwana wa Maaseya,
mwana wa Ithieli, mwana wa Yeshaya
8 na wafuasi wake, Gabai na Salai watu
928. 9 Yoeli mwana wa Zikri alikuwa
afisa wao mkuu, naye Yuda mwana
wa Hasenua alikuwa msimamizi juu
ya Mtaa wa Pili katika mji.

10 [a]Kutoka makuhani:
Yedaya, mwana wa Yoyaribu, Yakini,
11 [b]Seraya mwana wa Hilkia, mwana wa
Meshulamu, mwana wa Sadoki, mwana
wa Merayothi, mwana wa Ahitubu,
msimamizi katika nyumba ya Mungu,
12 pamoja na wenzao waliofanya kazi
hekaluni: watu 822. Adaya mwana wa
Yerohamu, mwana wa Pelalia, mwana
wa Amsi, mwana wa Zekaria, mwana
wa Pashuri, mwana wa Malkiya, 13 na
wenzao, waliokuwa viongozi wa
jamaa: watu 242. Amashisai mwana
wa Azareli, mwana wa Azai, mwana
wa Meshilemothi, mwana wa Imeri,
14 na wenzao waliokuwa wenye uwezo:
watu 128. Afisa wao mkuu alikuwa
Zabdieli mwana wa Hagedolimu.

15 Kutoka Walawi:
Shemaya mwana wa Hashubu, mwana
wa Azrikamu, mwana wa Hashabia,
mwana wa Buni; 16 [c]Shabethai
na Yozabadi, viongozi wawili wa
Walawi, ambao walisimamia kazi za
nje za nyumba ya Mungu; 17 [d]Matania
mwana wa Mika, mwana wa Zabdi,
mwana wa Asafu, kiongozi aliyeongoza
kutoa shukrani na maombi; Bakbukia
aliyekuwa msaidizi wake kati ya
wenzake; na Abda mwana wa
Shamua, mwana wa Galali, mwana
wa Yeduthuni. 18 [e]Jumla ya Walawi
waliokaa katika mji mtakatifu
walikuwa watu 284.

19 [f]Mabawabu:
Akubu, Talmoni na wenzao, waliolinda
malango: watu 172.

20 Waisraeli waliosalia, pamoja na
makuhani na Walawi, walikuwa katika miji
yote ya Yuda, kila mmoja katika urithi wa
baba yake.
21 [g]Watumishi wa Hekalu waliishi katika
kilima cha Ofeli. Siha na Gishpa walikuwa
wasimamizi wao.
22 [h]Afisa mkuu wa Walawi huko
Yerusalemu alikuwa Uzi mwana wa Bani,
mwana wa Hashabia, mwana wa Matania,
mwana wa Mika. Uzi alikuwa mmoja wa
wazao wa Asafu, waliokuwa waimbaji
wenye kuwajibika kwa ajili ya huduma ya
nyumba ya Mungu. 23 [i]Waimbaji walikuwa
chini ya amri za mfalme, ambazo pia
ziliratibu shughuli zao za kila siku.
24 [j]Pethahia mwana wa Meshezabeli,
mmoja wa wazao wa Zera mwana wa Yuda,
alikuwa mwakilishi wa mfalme katika
mambo yote kuhusu mahusiano na watu.
25 [k]Kuhusu vijiji na mashamba yake,
baadhi ya watu wa Yuda waliishi Kiriath-
Arba na makazi yaliyokizunguka, katika
Diboni na makazi yake, katika Yekabzeeli
na vijiji vyake, 26 [l]katika Yeshua, katika
Molada, katika Beth-Peleti, 27 [m]katika Hasar-
Shuali, katika Beer-Sheba na makazi yake,
28 [n]katika Siklagi, katika Mekona na makazi
yake, 29 [o]katika En-Rimoni, katika Sora,
katika Yarmuthi, 30 [p]Zanoa, Adulamu na
vijiji vyake, katika Lakishi na mashamba
yake, na katika Azeka na makazi yake.
Hivyo walikuwa wakiishi kuanzia Beer-
Sheba mpaka Bonde la Hinomu.
31 [q]Wazao wa Wabenyamini kutoka
Geba waliishi Mikmashi, Aiya, Betheli na

[a]**11:10** 1Nya 9:10
[b]**11:11** 2Fal 25:18; Ezr 7:2
[c]**11:16** Ezr 10:15; 2Nya 34:13; Ezr 8:33
[d]**11:17** 1Nya 9:15; Neh 12:8; 2Nya 5:12
[e]**11:18** Ufu 21:2; Ezr 9:8; Mt 24:15
[f]**11:19** 1Nya 9:17; Neh 7:45; 12:25
[g]**11:21** Ezr 2:43; Neh 3:26; 2Nya 27:3
[h]**11:22** 1Nya 9:15
[i]**11:23** 1Nya 15:16; Neh 7:44
[j]**11:24** Mwa 38:30; 1Nya 23:28
[k]**11:25** Mwa 35:27; Yos 14:15; Hes 21:30
[l]**11:26** Yos 15:27
[m]**11:27** Mwa 21:14
[n]**11:28** Isa 27:6
[o]**11:29** Yos 15:33-35; Yer 10:3
[p]**11:30** Yos 10:39; 10:10; 15:28
[q]**11:31** Yos 21:17; Isa 10:29; 1Sam 13:2

makazi yake, 32 [a]katika Anathothi, Nobu na
Anania, 33 [b]katika Hazori, Rama na Gitaimu,
34 [c]katika Hadidi, Seboimu na Nebalati,
35 [d]katika Lodi na Ono, na katika Bonde la
Mafundi.
36 Baadhi ya makundi ya Walawi wa Yuda
waliishi huko Benyamini.

*Makuhani Na Walawi Waliorudi Na Zerubabeli*

12 [e]Hawa wafuatao walikuwa makuhani
na Walawi ambao walirudi na
Zerubabeli mwana wa Shealtieli pamoja
na Yeshua:

Seraya, Yeremia, Ezra,
2 Amaria, Maluki, Hatushi,
3 Shekania, Rehumu, Meremothi,
4 [f]Ido, Ginethoni, Abiya,
5 Miyamini, Moadia, Bilga,
6 [g]Shemaya, Yoyaribu, Yedaya,
7 [h]Salu, Amoki, Hilkia na Yedaya.

Hawa walikuwa viongozi wa makuhani na
wenzao wakati wa Yeshua.
8 [i]Walawi walikuwa Yeshua, Binui,
Kadmieli, Sherebia, Yuda, na pia Matania,
ambaye pamoja na wenzake, alikuwa
kiongozi wa nyimbo za shukrani. 9 Bakbukia
na Uni, wenzao, walisimama mkabala nao
wakati wa ibada.
10 [j]Yeshua alikuwa baba wa Yoyakimu,
Yoyakimu alikuwa baba wa Eliashibu,
Eliashibu alikuwa baba wa Yoyada,
11 Yoyada alikuwa baba wa Yonathani, na
Yonathani alikuwa baba wa Yadua.
12 Katika siku za Yoyakimu, kulikuwa na
wakuu wa jamaa za kikuhani:

wa jamaa ya Seraya, Meraya;
wa jamaa ya Yeremia, Hanania;
13 wa jamaa ya Ezra, Meshulamu;
wa jamaa ya Amaria, Yehohanani;
14 wa jamaa ya Maluki, Yonathani;
wa jamaa ya Shebania, Yosefu;
15 wa jamaa ya Harimu, Adna;
wa jamaa ya Meremothi, Helkai;
16 [k]wa jamaa ya Ido, Zekaria;
wa jamaa ya Ginethoni, Meshulamu;
17 [l]wa jamaa ya Abiya, Zikri;
wa jamaa ya Miniamini na ya
Maazia, Piltai;
18 wa jamaa ya Bilgai, Shamua;
wa jamaa ya Shemaya, Yehonathani;
19 wa jamaa ya Yoyaribu, Matenai;
wa jamaa ya Yedaya, Uzi;
20 wa jamaa ya Salu, Kalai;
wa jamaa ya Amoki, Eberi;
21 wa jamaa ya Hilkia, Hashabia;
wa jamaa ya Yedaya, Nethaneli.

22 Wakuu wa jamaa za Walawi katika siku
za Eliashibu, Yoyada, Yohanani na Yadua,
pia wale jamaa za makuhani, waliandikishwa
wakati wa utawala wa Dario, Mwajemi.
23 [m]Wakuu wa jamaa miongoni mwa wazao
wa Lawi hadi wakati wa Yohanani mwana
wa Eliashibu waliandikishwa katika
kitabu cha kumbukumbu. 24 [n]Viongozi wa
Walawi walikuwa: Hashabia, Sherebia,
Yeshua mwana wa Kadmieli na wenzao,
waliosimama mkabala nao kusifu na
kushukuru, sehemu moja ikipokezana na
nyingine kama ilivyoagizwa na Daudi mtu
wa Mungu.
25 Mabawabu waliokuwa wakilinda
kwenye malango ya ghala ni: Matania,
Bakbukia, Obadia, Meshulamu, Talmoni na
Akubu. 26 [o]Walihudumu siku za Yoyakimu
mwana wa Yeshua, mwana wa Yosadaki,
na katika siku za mtawala Nehemia, na za
Ezra kuhani na mwandishi.

*Kuwekwa Wakfu Ukuta Wa Yerusalemu*

27 [p]Wakati wa kuwekwa wakfu ukuta
wa Yerusalemu, Walawi walitafutwa kule
walikokuwa wakiishi, nao wakaletwa

[a]**11:32** Isa 10:30; 1Sam 21:1
[b]**11:33** Yos 11:1; 18:25; 2Sam 4:3
[c]**11:34** 1Sam 13:18
[d]**11:35** 1Nya 8:12; 4:14
[e]**12:1** Neh 10:2-8; Zek 4:6-10; Ezr 3:2
[f]**12:4** Lk 1:5; 1Nya 24:10
[g]**12:6** 1Nya 24:7
[h]**12:7** Hag 1:1; Zek 5:1; Ezr 3:2
[i]**12:8** Neh 11:17; 1Nya 16:8
[j]**12:10** Ezr 10:24; Neh 3:20
[k]**12:16** Neh 12:4
[l]**12:17** 1Nya 24:10
[m]**12:23** 1Nya 9:14
[n]**12:24** Ezr 2:40; 3:11; 1Nya 23:1
[o]**12:26** Neh 8:9; Ezr 7:6, 11
[p]**12:27** Kum 20:5; 2Sam 6:5; 1Nya 25:6; Za 81:1-3; 92:3

Yerusalemu kuadhimisha kwa shangwe huko kuweka wakfu kwa nyimbo za shukrani na kwa uimbaji wakitumia matoazi, vinubi na zeze. 28 [a]Pia waimbaji walikusanywa pamoja kutoka maeneo yaliyozunguka Yerusalemu, kutoka vijiji vya Wanetofathi, 29 kutoka Beth-Gilgali, na kutoka eneo la Geba na Azmawethi, kwa kuwa waimbaji walikuwa wamejijengea vijiji kuzunguka Yerusalemu. 30 [b]Wakati makuhani na Walawi walipokuwa wamekwisha kujitakasa kwa kufuatana na desturi, waliwatakasa watu, malango na ukuta.

31 [c]Niliwaagiza viongozi wa Yuda wapande juu ya ukuta. Pia niliagiza makundi mawili makubwa ya waimbaji waimbe nyimbo za kumshukuru Mungu. Kundi moja lilipanda juu ya ukuta upande wa kuume, kuelekea Lango la Samadi. 32 Hoshaya na nusu ya viongozi wa Yuda wakawafuata, 33 pamoja na Azaria, Ezra, Meshulamu, 34 [d]Yuda, Benyamini, Shemaya, Yeremia, 35 [e]pamoja na baadhi ya makuhani wenye tarumbeta, na pia walikuwa na Zekaria mwana wa Yonathani, mwana wa Shemaya, mwana wa Matania, mwana wa Mikaya, mwana wa Zakuri, mwana wa Asafu, 36 [f]pamoja na wenzake, Shemaya, Azareli, Milalai, Gilalai, Maai, Nethaneli, Yuda na Hanani, wakiwa na vyombo vya uimbaji, kama ilivyoagizwa na Daudi mtu wa Mungu. Mwandishi Ezra aliongoza maandamano. 37 [g]Kwenye Lango la Chemchemi waliendelea moja kwa moja mpaka kwenye ngazi za Mji wa Daudi, kwenye mwinuko wa ukuta, na kupitia juu ya nyumba ya Daudi mpaka kwenye Lango la Maji upande wa mashariki.

38 [h]Kundi la pili la waimbaji lilielekea upande wa kushoto. Niliwafuata juu ya ukuta, pamoja na nusu ya watu kupitia Mnara wa Tanuru mpaka kwenye Ukuta Mpana, 39 [i]juu ya Lango la Efraimu, Lango la Yeshana, Lango la Samaki, Mnara wa Hananeli, na Mnara wa Mia, mpaka kwenye Lango la Kondoo. Walipofika kwenye Lango la Ulinzi wakasimama.

40 [j]Kisha yale makundi mawili ya waimbaji yaliyoshukuru yakachukua nafasi zao katika nyumba ya Mungu. Nami pia nikafanya hivyo, pamoja na nusu ya maafisa, 41 na makuhani wafuatao: Eliakimu, Maaseya, Miniamini, Mikaya, Elioenai, Zekaria na Hanania wakiwa na tarumbeta zao, 42 na pia Maaseya, Shemaya, Eleazari, Uzi, Yehohanani, Malkiya, Elamu na Ezeri. Makundi haya yaliimba chini ya uongozi wa Yezrahia. 43 [k]Siku hiyo watu walitoa dhabihu nyingi, wakishangilia kwa sababu Mungu aliwapa furaha kuu. Wanawake na watoto walishangilia pia. Sauti ya kushangilia huko Yerusalemu iliweza kusikika mbali sana.

44 [l]Wakati huo watu walichaguliwa kuwa wasimamizi wa vyumba vya ghala kwa ajili ya matoleo, malimbuko na zaka. Kutoka kwenye yale mashamba yaliyozunguka miji walipaswa walete kwenye ghala mafungu kama sheria ilivyoamuru kwa ajili ya makuhani na Walawi, kwa kuwa Yuda alifurahishwa na huduma ya makuhani na Walawi. 45 [m]Walifanya ibada ya Mungu wao na ibada ya utakaso, nao waimbaji na walinzi wa lango wakafanya hivyo pia, kufuatana na amri za Daudi na Solomoni mwanawe. 46 [n]Muda mrefu uliopita, katika siku za Daudi na Asafu, walikuwepo viongozi wa waimbaji na wa nyimbo za sifa na za kumshukuru Mungu. 47 [o]Kwa hiyo katika siku za Zerubabeli na za Nehemia, Israeli wote walitoa mafungu kila siku kwa ajili ya waimbaji na mabawabu. Pia walitenga fungu kwa ajili ya Walawi

[a]**12:28** 1Nya 2:54; 9:16
[b]**12:30** Kut 19:10; Ay 1:5
[c]**12:31** Neh 2:13; Ezr 3:10; Hes 10:2; 2Nya 5:12
[d]**12:34** Ezr 1:5
[e]**12:35** Ezr 3:10
[f]**12:36** 1Nya 23:5; 15:16; 2Nya 8:14
[g]**12:37** Neh 2:14; 3:3-15; 3:26; 2Sam 5:7-9
[h]**12:38** Neh 3:8-11
[i]**12:39** 2Fal 14:13; Neh 8:16; 2Nya 33:14; Neh 3:1-6
[j]**12:40** Za 42:4
[k]**12:43** Za 9:2; 92:4
[l]**12:44** Neh 13:4, 13; Law 27:30; Kum 18:8
[m]**12:45** 1Nya 25:1; 2Nya 8:14; 1Nya 6:31; 23:5
[n]**12:46** 2Nya 35:15; 29:27
[o]**12:47** Hes 18:21; Kum 18:8

wengine, nao Walawi walitenga fungu kwa
ajili ya wazao wa Aroni.

*Nehemia Afanya Matengenezo Ya Mwisho*

13 [a]Siku hiyo, Kitabu cha Mose kilisomwa
kwa sauti kuu, na watu wote
wakasikia. Humo ilionekana imeandikwa
kwamba hakuna Mwamoni wala Mmoabu
atakayeruhusiwa katika kusanyiko la watu
wa Mungu, 2 [b]kwa sababu hawakuwalaki
Waisraeli kwa chakula na maji. Badala yake
walimwajiri Balaamu kuwalaani (lakini
hata hivyo Mungu wetu aligeuza laana
kuwa baraka). 3 [c]Watu waliposikia sheria
hii, waliwatenga watu wote wasio Waisraeli
waliokuwa wa uzao wa kigeni.
4 [d]Kabla ya hili, kuhani Eliashibu alikuwa
amewekwa kuwa msimamizi wa vyumba
vya ghala ya nyumba ya Mungu wetu.
Alikuwa na uhusiano wa karibu na Tobia,
5 [e]naye alikuwa amempa Tobia chumba
kikubwa ambacho mwanzo kilikuwa
kikitumika kuweka sadaka za nafaka,
uvumba na vyombo vya Hekalu, pamoja
na zaka za nafaka, divai mpya na mafuta
waliyoagizwa Waisraeli kwa ajili ya Walawi,
waimbaji na mabawabu wa lango, pamoja
na matoleo kwa makuhani.
6 [f]Lakini wakati haya yote yalipokuwa
yakitendeka, sikuwa Yerusalemu, kwa
kuwa katika mwaka wa thelathini na
mbili wa utawala wa Artashasta mfalme
wa Babeli nilikuwa nimerudi kwa mfalme.
Baadaye nilimwomba ruhusa, 7 [g]nikarudi
Yerusalemu. Hapo niligundua jambo la
uovu alilofanya Eliashibu kwa kumpa
Tobia chumba katika nyua za nyumba ya
Mungu. 8 [h]Nilikasirika sana na nikavitupa
nje vyombo vyote vya Tobia. 9 [i]Nilitoa amri
kutakasa vyumba, kisha nikavirudisha vifaa
vya nyumba ya Mungu, pamoja na sadaka
za nafaka na uvumba.
10 [j]Pia niligundua kuwa mafungu
yaliyopangwa kupewa Walawi hawakuwa
wamepewa, nao Walawi wote na waimbaji
waliowajibika kwa huduma walikuwa
wamerudi katika mashamba yao. 11 [k]Basi
niliwakemea maafisa na kuwauliza, “Kwa
nini nyumba ya Mungu imepuuzwa?” Kisha
niliwaita pamoja na kuwaweka kwenye
nafasi zao.
12 [l]Yuda wote walileta zaka za nafaka,
divai mpya na mafuta kwenye ghala.
13 [m]Nikamweka kuhani Shelemia, mwandishi
Sadoki, na Mlawi aliyeitwa Pedaya kuwa
wasimamizi wa ghala, na kumfanya Hanani
mwana wa Zakuri, mwana wa Matania
kuwa msaidizi wao, kwa sababu watu hawa
walionekana kuwa waaminifu. Walipewa
wajibu wa kugawa mahitaji kwa ndugu zao.

14 [n]Ee Mungu wangu, unikumbuke kwa
hili, wala usifute kile nilichokifanya kwa
uaminifu kwa ajili ya nyumba ya Mungu
wangu na kwa ajili ya huduma yake.

15 [o]Siku hizo nikaona watu katika Yuda
wakikanyaga mashinikizo ya divai siku
ya Sabato na kuleta nafaka wakiwapakiza
punda, pamoja na divai, zabibu, tini na aina
nyingine za mizigo. Nao walikuwa wakileta
haya yote Yerusalemu siku ya Sabato. Kwa
hiyo niliwaonya dhidi ya kuuza vyakula
siku hiyo. 16 [p]Watu kutoka Tiro waliokuwa
wakiishi Yerusalemu walileta samaki
na aina nyingi za bidhaa na kuziuza
Yerusalemu siku ya Sabato kwa watu wa
Yuda. 17 [q]Niliwakemea wakuu wa Yuda na
kuwaambia, “Ni uovu gani huu mnaofanya
wa kuinajisi siku ya Sabato? 18 [r]Je, baba
zenu hawakufanya mambo kama haya, hata
wakamsababisha Mungu wetu kuleta maafa

[a]**13:1** Amo 2:1-3; Kum 23:3
[b]**13:2** Hes 22:3-11; 23:7; 23:8-11; Kum 23:3-5
[c]**13:3** Neh 9:2; Yak 1:27
[d]**13:4** Neh 12:44; 2:10
[e]**13:5** Law 27:30; Hes 18:21
[f]**13:6** Neh 5:14; 2:6
[g]**13:7** Ezr 10:24
[h]**13:8** Mk 11:15-17; Yn 2:13; Lk 19:45-46
[i]**13:9** 1Nya 23:28; 2Nya 29:5
[j]**13:10** Kum 12:19; Hes 35:2
[k]**13:11** Hag 1:9; 1Sam 2:17; Mal 3:8-9
[l]**13:12** Kum 18:8; 2Nya 31:5-6
[m]**13:13** Neh 12:44; Mdo 6:1-5
[n]**13:14** Neh 5:19; Mwa 8:1; 2Fal 20:3
[o]**13:15** Kut 34:21; Kum 5:12-15
[p]**13:16** Neh 10:31
[q]**13:17** Neh 13:11
[r]**13:18** Neh 10:31; Yer 17:21-23

haya yote juu yetu na juu ya mji huu? Sasa
bado mnazidi kuchochea ghadhabu yake
dhidi ya Israeli kwa kuinajisi Sabato."
19 [a]Wakati vivuli vya jioni vilipoangukia
juu ya malango ya Yerusalemu kabla
ya Sabato, niliamuru milango ifungwe,
wala isifunguliwe mpaka Sabato iishe.
Nikawaweka baadhi ya watu wangu
mwenyewe kwenye malango ili pasiwepo
mzigo utakaoingizwa ndani siku ya
Sabato. 20 Mara moja au mbili wachuuzi
na wauzaji wa bidhaa za aina zote walilala
usiku nje ya mji wa Yerusalemu. 21 Lakini
niliwaonya na kuwaambia, "Kwa nini
mnalala karibu na ukuta? Kama mkifanya
hivi tena, nitawaadhibu." Kuanzia wakati
ule hawakuja tena siku ya Sabato. 22 [b]Kisha
nikawaamuru Walawi kujitakasa na kwenda
kulinda malango ili kutunza Sabato iwe
takatifu.

Ee Mungu wangu, unikumbuke kwa ajili ya hili pia, nawe unionyeshe wema wako sawasawa na upendo wako mkuu.

23 [c]Zaidi ya hayo, niliona Wayahudi
waliokuwa wameoa wanawake kutoka
Ashdodi, Amoni na Moabu. 24 [d]Nusu ya
watoto wao walizungumza lugha ya
Kiashidodi au lugha ya watu wengine,
bali hawakuweza kuzungumza Kiyahudi.
25 [e]Niliwakemea na kuwalaani. Niliwapiga
baadhi ya watu na kung'oa nywele zao.
Niliwaapisha kwa jina la Mungu na kusema:
"Msiwaoze binti zenu kwa wana wao, wala
binti zao wasiolewe na wana wenu wala
ninyi wenyewe. 26 [f]Je, Solomoni hakutenda
dhambi kwa sababu ya wanawake wa
namna hiyo? Miongoni mwa mataifa
mengi hapakuwepo mfalme kama yeye.
Alipendwa na Mungu wake. Naye Mungu
alimweka kuwa mfalme juu ya Israeli yote,
lakini hata yeye, wanawake wa mataifa
mengine walimfanya atende dhambi. 27 [g]Je,
tulazimike sasa kusikia kwamba ninyi pia
mmefanya uovu huu mkubwa na kutokuwa
waaminifu kwa Mungu wetu kwa kuoa
wanawake wa kigeni?"
28 [h]Mmoja wa wana wa Yoyada mwana wa
Eliashibu kuhani mkuu alikuwa mkwewe
Sanbalati Mhoroni. Nami nilimfukuza
mbele yangu.

29 [i]Ee Mungu wangu, uwakumbuke, kwa
sababu wamenajisi ukuhani, na agano la
kikuhani na la Walawi.

30 [j]Kwa hiyo niliwatakasa makuhani na
Walawi kutokana na chochote kilichokuwa
cha kigeni, na kuwapa wajibu, kila mmoja
katika kazi yake. 31 [k]Pia nilihakikisha
kwamba matoleo ya kuni yaliletwa kwa
wakati unaopaswa, na malimbuko kwa
wakati wake.

Ee Mungu wangu, unikumbuke, unitendee mema.

[a]**13:19** Law 23:32; Kut 31:14-17
[b]**13:22** Mwa 8:1; Neh 1:8
[c]**13:23** Neh 12:30; Ezr 9:1-2; Mal 2:11; Kut 34:16; Rut 1:4
[d]**13:24** Es 1:22; 3:12; 8:9
[e]**13:25** Ezr 10:5; Mit 28:4; Neh 10:29-30
[f]**13:26** 1Fal 3:13; 2Nya 1:12
[g]**13:27** Ezr 9:14; 10:2
[h]**13:28** Ezr 10:24; Neh 10:30
[i]**13:29** Neh 10:34; Mwa 8:1; Neh 1:8
[j]**13:30** Neh 9:2
[k]**13:31** Neh 10:34; 10:35-36; Mwa 8:1; Neh 1:8

# ESTA

*Malkia Vashti Aondolewa*

1 [a]Hili ndilo lililotokea wakati wa utawala wa Mfalme Ahasuero, yule aliyetawala juu ya majimbo mia na ishirini na saba tangu Bara Hindi hadi Kushi.[b] 2 Wakati huo Mfalme Ahasuero alitawala katika kiti chake cha enzi katika ngome ya mji wa Shushani. 3 [c]Katika mwaka wa tatu wa utawala wake, alifanya karamu kwa ajili ya wakuu wake wote pamoja na maafisa. Akawaalika viongozi wa jeshi wa Uajemi na Umedi, wana wa wafalme na wakuu wa majimbo.

4 Kwa siku zote 180 mfalme alionyesha utajiri mwingi wa ufalme wake, fahari na utukufu wa enzi yake. 5 [d]Siku hizo zilipopita, mfalme alifanya karamu kwa muda wa siku saba, katika bustani ya ndani katika jumba la kifalme, kwa ajili ya watu wote kuanzia mdogo hadi mkubwa, waliokuwa katika ngome ya mji wa Shushani. 6 [e]Bustani ilikuwa na mapazia ya kitani nyeupe na buluu, yaliyofungiwa kamba za kitani nyeupe na kitambaa cha zambarau, kwenye pete za fedha juu ya nguzo za marmar. Kulikuwepo viti vya dhahabu na vya fedha vilivyokuwa vimewekwa kwenye ile sakafu iliyotengenezwa kwa mawe ya rangi, marmar, lulumizi na mawe mengine ya thamani. 7 Vyombo vya dhahabu vilitumika kwa watu kunywea mvinyo, kila kimoja tofauti na kingine, naye mfalme akatoa mvinyo kwa wingi kwa kadiri ya ukarimu wake. 8 Kwa amri ya mfalme kila mgeni aliruhusiwa kunywa alichotaka, kwa kuwa mfalme alitoa maagizo kwa watumishi wote wa kuhudumu mvinyo kumhudumia kila mtu kwa jinsi alivyotaka.

9 Malkia Vashti pia akawafanyia wanawake karamu katika jumba la kifalme la Mfalme Ahasuero.

10 [f]Siku ya saba, wakati Mfalme Ahasuero alikuwa amesisimka roho yake kwa mvinyo, aliamuru matowashi saba waliokuwa wakimhudumia, yaani, Mehumani, Biztha, Harbona, Bigtha, Abagtha, Zethari na Karkasi, 11 kumleta Malkia Vashti mbele ya mfalme akiwa amevaa taji lake la kifalme, ili aonyeshe uzuri wake kwa watu na wakuu, kwa kuwa alikuwa ni mzuri wa kupendeza. 12 [g]Lakini wakati watumishi walipotoa amri ya mfalme, Malkia Vashti alikataa kuja. Ndipo mfalme alighadhibika, na hasira yake ikawaka.

13 [h]Kwa kuwa ilikuwa desturi ya mfalme kupata ushauri kwa wataalamu katika mambo ya sheria na haki, alizungumza na watu wenye busara, ambao walijua nyakati, 14 nao waliokuwa karibu na mfalme ni Karshena, Shethari, Admatha, Tarshishi, Meresi, Marsena na Memukani, wakuu saba wa Uajemi na Umedi waliokuwa na nafasi ya pekee kwa mfalme nao walikuwa na vyeo vya juu kabisa katika utawala wake.

15 Mfalme akauliza, “Kulingana na sheria, Malkia Vashti anapaswa kutendewa nini? Malkia hakutii amri ya Mfalme Ahasuero ambayo matowashi walimpelekea.”

16 Kisha Memukani akajibu mbele ya mfalme na wakuu, “Malkia Vashti si kwamba amemkosea mfalme tu bali pia amewakosea wakuu wote na watu wa himaya yote ya Mfalme Ahasuero. 17 Kwa maana tendo hili la malkia litajulikana kwa wanawake wote, kwa hiyo watawadharau waume zao na kusema, ‘Mfalme Ahasuero aliagiza Malkia Vashti aletwe mbele yake, lakini alikataa.’ 18 Leo hii wanawake wa wakuu wa Uajemi na Umedi ambao wamesikia juu ya tabia ya malkia watawatendea wakuu wote wa mfalme vivyo hivyo. Hapatakuwepo na mwisho wa dharau na magomvi.

19 [i]“Kwa hiyo, kama itampendeza mfalme,

[a]**1:1** Ezr 4:16; Es 9:30
[b]1 Kushi hapa ina maana ya Ethiopia.
[c]**1:3** 1Fal 3:15
[d]**1:5** Amu 14:17; 2Fal 21:18
[e]**1:6** Eze 23:41; Amo 3:12; 6:4
[f]**1:10** Rut 3:7; Dan 5:1-4
[g]**1:12** Mwa 39:19; Mit 19:12
[h]**1:13** 1Nya 12:32
[i]**1:19** Es 8:6; Dan 6:8, 12

atoe amri ya kifalme na iandikwe katika sheria ya Uajemi na Umedi, ambayo haitabadilika, kwamba Vashti kamwe asije tena mbele ya Mfalme Ahasuero. Pia mfalme na atoe hiyo nafasi yake ya umalkia kwa mwanamke mwingine aliye bora kumliko yeye. [20] Kisha mbiu hii ya mfalme itakapotangazwa katika himaya yake iliyo kubwa sana, wanawake wote watawaheshimu waume zao, kuanzia mdogo hadi mkubwa."

[21] Mfalme na wakuu wake walipendezwa na shauri hili, hivyo basi mfalme akafanya kama Memukani alivyopendekeza. [22] [a]Alipeleka barua katika sehemu zote za ufalme wake, kwa kila jimbo kwa maandishi yake mwenyewe na kwa kila watu katika lugha yao wenyewe, akitangaza kwa msemo wa kila watu kwamba inampasa kila mwanaume kuwa mtawala wa nyumba yake mwenyewe.

*Esta Afanywa Malkia*

2 Baadaye, wakati hasira ya Mfalme Ahasuero ilikuwa imetulia, alimkumbuka Vashti na kile alichokuwa amekifanya na alilokuwa ameamuru juu yake. [2] Kisha watumishi waliomhudumia mfalme walipendekeza, "Na ufanyike utafiti kwa ajili ya wanawali mabikira wazuri wa sura kwa ajili ya mfalme. [3] Mfalme na ateue maafisa katika kila jimbo la himaya yake kuwaleta hao wanawali wote wazuri wa sura katika nyumba ya wanawake katika ngome ya mji wa Shushani. Kisha wawekwe chini ya utunzaji wa Hegai, towashi wa mfalme, msimamizi wa wanawake; na wapewe matunzo yote ya urembo. [4] Kisha yule ambaye atampendeza mfalme na awe malkia badala ya Vashti." Shauri hili likampendeza mfalme, naye akalifuata.

[5] [b]Basi katika mji wa ngome ya Shushani palikuwa na Myahudi wa kabila ya Benyamini, jina lake Mordekai mwana wa Yairi, mwana wa Shimei, mwana wa Kishi, [6] [c]ambao walichukuliwa uhamishoni kutoka Yerusalemu na Mfalme Nebukadneza wa Babeli, wakiwa miongoni mwa waliochukuliwa mateka pamoja na Mfalme Yekonia wa Yuda. [7] [d]Mordekai alikuwa na binamu yake msichana aliyeitwa Hadasa, ambaye alimlea kwa kuwa hakuwa na baba wala mama. Msichana huyu, ambaye pia alijulikana kwa jina la Esta, alikuwa na umbo na sura ya kupendeza, naye Mordekai alimtunza kama binti yake mwenyewe baada ya baba yake na mama yake kufariki.

[8] Wakati agizo na amri ya mfalme lilitangazwa, wanawali wengi waliletwa kwenye ngome ya mji wa Shushani na kuwekwa chini ya uangalizi wa Hegai. Pia Esta alipelekwa katika jumba la mfalme na akakabidhiwa Hegai, aliyekuwa mkuu wa nyumba ya wanawake. [9] [e]Msichana huyu alimpendeza na kupata kibali mbele zake. Mara moja akaanza kumpa matunzo ya uzuri na chakula maalum. Alimpa Esta vijakazi saba waliochaguliwa kutoka jumba la kifalme, na kumhamishia yeye pamoja na vijakazi wake katika sehemu bora zaidi katika nyumba ya wanawake.

[10] [f]Esta alikuwa hajadhihirisha uraia wala kabila lake, kwa sababu Mordekai alikuwa amemkataza. [11] Kila siku Mordekai alikuwa akitembeatembea karibu na ua wa nyumba ya wanawake kujua Esta alivyoendelea na kuona yaliyokuwa yakitendeka kwake.

[12] [g]Kabla zamu ya msichana haijafika ya kwenda kwa Mfalme Ahasuero, ilimbidi atimize miezi kumi na miwili ya matunzo ya urembo kama ilivyokuwa imepangwa. Kwa miezi sita walikuwa wajipake mafuta ya manemane, na miezi sita kujipaka manukato na vipodozi. [13] Basi hivi ndivyo ambavyo msichana angeingia kwa mfalme: Kila kitu alichohitaji aliruhusiwa kuchukua kutoka nyumba ya wanawake na kwenda navyo katika jumba la mfalme. [14] [h]Jioni angekwenda pale na asubuhi kurudi sehemu nyingine ya nyumba ya wanawake katika utunzaji wa Shaashgazi, towashi wa mfalme ambaye alikuwa mkuu wa masuria.

---

[a]**1:22** Neh 13:24
[b]**2:5** 1Sam 9:1
[c]**2:6** 2Fal 24:15
[d]**2:7** Mwa 41:45; 39:6
[e]**2:9** 1Sam 9:22-24; Eze 16:9-13
[f]**2:10** Es 2:20
[g]**2:12** Mit 27:9; Isa 3:24
[h]**2:14** 1Fal 11:3; Dan 5:2

Hangeweza kurudi kwa mfalme mpaka apendezwe naye na kuagiza aitwe kwa jina lake.

15 [a]Zamu ya Esta ilipofika kwenda kwa mfalme (msichana ambaye Mordekai alikuwa amemlea, binti wa Abihaili mjomba wake), Esta hakutaka vitu zaidi ya vile ambavyo Hegai, towashi wa mfalme aliyekuwa mkuu wa nyumba ya wanawake alivyokuwa amemshauri. Naye Esta alipata kibali kwa kila mtu aliyemwona.
16 Esta alipelekwa kwa Mfalme Ahasuero katika makao ya mfalme mwezi wa kumi, yaani mwezi wa Tebethi, katika mwaka wake wa saba wa kutawala.

17 Basi ikawa mfalme alivutiwa na Esta kuliko wanawake wengine wote, naye akapata upendeleo na kibali kuliko mabikira wengine. Kisha akamvika taji la kifalme kichwani mwake na kumfanya malkia badala ya Vashti.
18 [b]Mfalme akafanya karamu kubwa, karamu ya Esta, kwa wakuu wake wote na maafisa. Mfalme alitangaza mapumziko katika majimbo yake yote na kugawa zawadi kwa ukarimu wa kifalme.

*Mordekai Afunua Hila*

19 [c]Wakati mabikira walikusanyika mara ya pili, Mordekai alikuwa ameketi katika lango la mfalme.
20 Lakini Esta alikuwa ameficha siri ya kabila lake na uraia wake, kama Mordekai alivyokuwa amemwambia, kwa maana aliendelea kufuata maelekezo ya Mordekai kama alivyokuwa akifanya alipokuwa akimlea.

21 Wakati Mordekai alikuwa ameketi kwenye lango la mfalme, Bigthana na Tereshi, maafisa wawili wa mfalme waliokuwa walinzi wa lango, walikasirika na kupanga njama ya kumuua Mfalme Ahasuero.
22 Lakini Mordekai aligundua hila hii na kumwambia Malkia Esta, ambaye baadaye alimwarifu mfalme, huku akimsifu Mordekai.
23 [d]Taarifa hiyo ilipochunguzwa na kuonekana kuwa kweli, maafisa hao wawili waliangikwa juu ya miti ya kunyongea. Haya yote yaliandikwa katika kitabu cha kumbukumbu mbele ya mfalme.

*Hila Ya Hamani Kuwaangamiza Wayahudi*

3 [e]Baada ya matukio haya, Mfalme Ahasuero alimheshimu Hamani mwana wa Hamedatha, Mwagagi, akampandisha na kumpa kiti chake cha heshima cha juu sana kuliko wakuu wengine wote.
2 [f]Maafisa wote wa mfalme waliokaa langoni mwa mfalme walipiga magoti na kumpa Hamani heshima, kwa kuwa mfalme alikuwa ameamuru hili kuhusu Hamani. Lakini Mordekai hakumpigia magoti wala kumheshimu.

3 Kisha maafisa wa mfalme waliokuwa langoni mwa mfalme walimuuliza Mordekai, "Kwa nini hutii agizo la mfalme?"
4 [g]Siku baada ya siku walizungumza naye lakini hakukubali. Kwa hiyo walimweleza Hamani kuona kama tabia ya Mordekai itaweza kuvumiliwa, kwa maana alikuwa amewaambia kuwa yeye ni Myahudi.

5 Wakati Hamani alipoona kuwa Mordekai hampigii magoti wala kumpa heshima alighadhibika.
6 [h]Hata hivyo baada ya kujulishwa watu wa Mordekai ni akina nani, alibadili wazo la kumuua Mordekai peke yake. Badala yake Hamani alitafuta njia ya kuwaangamiza watu wote wa Mordekai, yaani, Wayahudi, walio katika ufalme wote wa Ahasuero.

7 [i]Katika mwaka wa kumi na mbili wa utawala wa Mfalme Ahasuero, katika mwezi wa kwanza uitwao Nisani, walipiga puri (yaani kura) mbele ya Hamani ili kuchagua siku na mwezi. Kura ikaangukia kwenye mwezi wa kumi na mbili, yaani Adari.

8 [j]Kisha Hamani akamwambia Mfalme Ahasuero, "Wako watu fulani wameenea na kutawanyika miongoni mwa watu katika majimbo yote ya ufalme wako, ambao desturi zao ni tofauti na zile za

---

[a]**2:15** Za 45:14; Mwa 18:3
[b]**2:18** 1Fal 3:15; Es 1:7
[c]**2:19** Es 4:2
[d]**2:23** Mwa 40:19; Mhu 10:8
[e]**3:1** Hes 24:7; 1Sam 14:48; Hes 24:7; 1Sam 14:48
[f]**3:2** Dan 3:12
[g]**3:4** Mwa 39:10
[h]**3:6** Mit 16:25; Za 74:8
[i]**3:7** Es 9:24, 26; 1Sam 10:21
[j]**3:8** Mdo 16:20-21; Ezr 4:15

watu wengine wote, nao hawatii sheria za
mfalme. Haifai mfalme kuwavumilia watu
hawa. 9 Kama inampendeza mfalme, itolewe
amri kuwaangamiza, nami nitaweka talanta
10,000[a] za fedha katika hazina ya mfalme
kwa ajili ya watu watakaoshughulikia
jambo hili.”

10 Basi mfalme alichukua pete yake ya
muhuri kutoka kwenye kidole chake na
kumpa Hamani mwana wa Hamedatha,
Mwagagi, adui wa Wayahudi. 11 Mfalme
akamwambia Hamani, “Baki na fedha yako
na uwatendee hao watu utakavyo.”

12 [b]Kisha siku ya kumi na tatu ya mwezi
wa kwanza waandishi wa mfalme waliitwa.
Wakaandika barua kwa kila jimbo na katika
kila lugha ya watu kama agizo la Hamani
lilivyotoka kwa mfalme, kwa watawala wa
majimbo mbalimbali, na wakuu wa watu
mbalimbali. Hizi ziliandikwa kwa jina la
Mfalme Ahasuero mwenyewe na kutiwa
muhuri wa pete yake mwenyewe. 13 [c]Barua
zilipelekwa na tarishi katika majimbo yote
ya mfalme zikiwa na amri ya kuharibu,
kuua na kuangamiza Wayahudi wote,
wadogo kwa wakubwa, wanawake na
watoto wadogo, siku moja, yaani siku ya
kumi na tatu ya mwezi wa kumi na mbili,
ndio mwezi wa Adari, na pia kuteka nyara
vitu vyao. 14 Nakala ya andiko la amri
ilipaswa kutolewa kama sheria katika kila
jimbo, na kufahamishwa kwa watu wa kila
taifa ili waweze kuwa tayari kwa siku ile.

15 [d]Kwa kuharakishwa na amri ya mfalme,
matarishi walikwenda na andiko lilitolewa
katika mji wa ngome ya Shushani. Mfalme
na Hamani waliketi na kunywa, lakini mji
wa Shushani ulifadhaika.

*Mordekai Amshawishi Esta Kusaidia*

4 [e]Mordekai alipojua yote yaliyokwisha
kufanyika, alirarua mavazi yake na
kuvaa nguo za magunia na kujipaka majivu,
akaenda mjini, akiomboleza kwa sauti na
kwa uchungu. 2 Alikwenda akasimama nje
ya lango la mfalme, kwa sababu hakuna
yeyote aliyeruhusiwa kuingia akiwa amevaa
nguo za magunia. 3 Katika kila jimbo
ambapo amri na agizo la mfalme lilifika,
kulikuwa na maombolezo makuu miongoni
mwa Wayahudi pamoja na kufunga, kulia
na kuomboleza. Watu wengi wakalala juu
ya nguo za magunia na majivu.

4 Wajakazi wa Esta na matowashi
walipokuja na kumwambia kuhusu
Mordekai, alipatwa na huzuni kuu.
Alimtumia nguo avae badala ya nguo za
magunia, lakini Mordekai hakuzikubali.
5 Ndipo Esta akamwita Hathaki, mmojawapo
wa matowashi wa mfalme ambaye alikuwa
amewekwa kumhudumia Esta, akamwagiza
kutafuta ni nini kilikuwa kikimtaabisha
Mordekai na ni kwa nini.

6 Basi Hathaki alitoka nje kumwendea
Mordekai kwenye uwanja ulio wazi wa
mji mbele ya lango la mfalme. 7 [f]Mordekai
akamwambia kila kitu ambacho kimempata,
pamoja na hesabu kamili ya fedha ambazo
Hamani aliahidi kulipa katika hazina
ya mfalme kwa ajili ya maangamizi ya
Wayahudi. 8 Akampa nakala ya andiko
la amri kwa ajili ya maangamizi yao,
lililokuwa limechapishwa huko Shushani,
kumwonyesha Esta na kumwelezea.
Mordekai akamwambia towashi amshawishi
Esta kwenda mbele ya mfalme kuomba
rehema na kumsihi kwa ajili ya watu wake.

9 Hathaki akarudi kwa Esta na kumwarifu
alilolisema Mordekai. 10 Kisha Esta
akamwamuru Hathaki amweleze Mordekai,
11 [g]“Maafisa wote wa mfalme na watu
wa majimbo ya ufalme wanajua kuwa
mwanaume au mwanamke yeyote ambaye
ataingia kumwona mfalme katika ua wa
ndani bila kuitwa, mfalme ana sheria moja
tu: Atauawa. Njia pekee kinyume na hili ni
mfalme kumnyooshea fimbo ya dhahabu ili
aishi. Lakini siku thelathini zimepita tangu
nilipoitwa kwenda kwa mfalme.”

12 Wakati Mordekai aliarifiwa maneno
ya Esta, 13 Mordekai alirudisha jibu hili:
“Usifikiri kwamba kwa sababu uko katika

---

[a]9 Talanta 10,000 za fedha ni sawa na tani 340.
[b]**3:12** Neh 13:24; Mwa 38:18
[c]**3:13** Es 8:11
[d]**3:15** Es 8:15
[e]**4:1** Eze 27:30-31; Za 30:11
[f]**4:7** Es 7:4
[g]**4:11** Dan 2:9; Za 125:3

nyumba ya mfalme wewe pekee katika
Wayahudi wote utapona. 14 [a]Kwa kuwa
kama utakaa kimya wakati huu, msaada
na ukombozi kwa Wayahudi utatoka mahali
pengine, lakini wewe na jamaa ya baba
yako mtaangamia. Nani ajuaye kwamba
hukuja kwenye nafasi ya mamlaka kwa ajili
ya wakati kama huu?”
15 Kisha Esta alituma jibu hili kwa
Mordekai: 16 [b]“Nenda, kusanya pamoja
Wayahudi wote walioko Shushani, nanyi
mfunge kwa ajili yangu. Msile wala
kunywa kwa siku tatu, usiku na mchana.
Mimi na wajakazi wangu tutafunga kama
mnavyofanya. Baada ya kufanyika hili,
nitakwenda kwa mfalme, hata ingawa ni
kinyume cha sheria. Ikiwa ni kuangamia
na niangamie.”
17 Kwa hiyo Mordekai alikwenda zake na
kutekeleza maagizo yote ya Esta.

### *Ombi La Esta Kwa Mfalme*

5 [c]Siku ya tatu, Esta alivaa mavazi yake
ya kimalkia, naye akasimama katika ua
wa ndani wa jumba la mfalme, mbele ya
ukumbi wa mfalme. Naye mfalme alikuwa
akiketi katika kiti chake cha kifalme katika
ukumbi, akielekea langoni. 2 Alipomwona
Malkia Esta amesimama uani alipendezwa
naye, akamnyooshea fimbo ya utawala ya
dhahabu ile iliyokuwa mkononi mwake.
Kwa hiyo Esta alikaribia na kuigusa ncha
ya fimbo ya mfalme.
3 [d]Kisha mfalme aliuliza, “Malkia Esta,
ni nini? Ombi lako ni nini? Hata kama ni
nusu ya ufalme, utapewa.”
4 Esta akajibu, “Kama itampendeza
mfalme, mfalme pamoja na Hamani waje
leo katika karamu ambayo nimeiandaa kwa
ajili yake.”
5 Mfalme akasema, “Mleteni Hamani
mara moja, ili tupate kufanya lile Esta
analoomba.”
Kwa hiyo mfalme na Hamani
walihudhuria karamu aliyoiandaa Esta.
6 [e]Walipokuwa wakinywa mvinyo mfalme
akamuuliza Esta tena, “Sasa haja yako ni
nini? Utapewa. Ombi lako ni nini? Hata
nusu ya ufalme, utapewa.”
7 Esta akajibu, “Haja yangu na ombi
langu ni hili: 8 [f]Kama mfalme ameona
vyema, nami nimepata kibali kwake na
kama ikimpendeza mfalme kunipa ombi
langu na kunitimizia haja yangu, mfalme na
Hamani waje kwangu kesho katika karamu
nitakayowaandalia. Kisha nitajibu swali la
mfalme.”

### *Ghadhabu Ya Hamani Dhidi Ya Mordekai*

9 [g]Hamani alitoka siku hiyo kwa furaha
na moyo mchangamfu. Lakini alipomwona
Mordekai langoni mwa mfalme na kuona
kwamba hakusimama wala hakuonyesha
hofu mbele yake, alijawa na ghadhabu
dhidi ya Mordekai. 10 [h]Hata hivyo, Hamani
alijizuia akaenda zake nyumbani.
Akawaita pamoja rafiki zake na Zereshi,
mkewe. 11 [i]Hamani akajisifia kwao juu ya
utajiri wake mwingi, wanawe wengi na kwa
njia zote ambazo mfalme amemheshimu
kwazo na jinsi alivyomweka juu ya wakuu
na maafisa wengine. 12 Hamani akaongeza,
“Si hayo tu. Mimi ndiye mtu pekee ambaye
Malkia Esta amemwalika kumsindikiza
mfalme kwenye karamu aliyomwandalia.
Naye amenialika pamoja na mfalme kesho.
13 Lakini haya yote hayanipi kuridhika
iwapo ninaendelea kumwona yule Myahudi
Mordekai akiketi kwenye lango la mfalme.”
14 [j]Zereshi mkewe na rafiki zake wote
wakamwambia, “Tengeneza mahali pa
kuangika watu kimo chake dhiraa hamsini,[k]
kisha kesho asubuhi mwombe mfalme
Mordekai aangikwe juu yake. Ndipo uende
na mfalme kwenye karamu kwa furaha.”
Shauri hili lilimpendeza Hamani, naye
akajenga mahali pa kuangika watu.

---

[a]**4:14** Ay 34:29; Mhu 3:7; Amo 5:13
[b]**4:16** 2Nya 20:3; Mwa 43:14
[c]**5:1** Eze 16:13; Mit 21:1
[d]**5:3** Es 7:2; Mk 6:23
[e]**5:6** Dan 5:16
[f]**5:8** Es 2:15; 1Fal 3:15
[g]**5:9** Mit 14:17
[h]**5:10** Es 6:13
[i]**5:11** Mit 13:16; Es 9:10, 13
[j]**5:14** Es 7:9; Ezr 6:11
[k]14 Dhiraa 50 ni sawa na mita 22.5.

*Mordekai Anapewa Heshima*

6 [a]Usiku ule mfalme hakupata usingizi,
hivyo akaagiza aletewe kitabu cha
kumbukumbu za matukio ya utawala
wake, asomewe. 2 Kitabu hicho kilikutwa na
kumbukumbu kwamba Mordekai alikuwa
amefichua jinsi Bigthana na Tereshi,
waliokuwa maafisa wawili wa mfalme,
walinzi wa lango walivyokuwa wamepanga
hila ya kumuua Mfalme Ahasuero.
3 [b]Mfalme akauliza, “Je, ni heshima na
shukrani gani Mordekai alipokea kwa ajili
ya jambo hili?”

Watumishi wake wakajibu, “Hakuna
lolote alilofanyiwa.”

4 Mfalme akasema, “Ni nani yuko uani?”
Wakati huo huo Hamani alikuwa ameingia
ua wa nje wa jumba la mfalme kusema na
mfalme kuhusu kumwangika Mordekai
katika mahali pa kuangikia watu alipokuwa
amepajenga kwa ajili yake.

5 Watumishi wake wakamjibu, “Hamani
amesimama uani.”

Mfalme akaamuru, “Mleteni ndani.”

6 Hamani alipoingia, mfalme alimuuliza,
“Afanyiwe nini mtu ambaye mfalme apenda
kumheshimu?”

Basi Hamani akawaza moyoni mwake,
“Ni nani mwingine ambaye mfalme
angemheshimu kuliko mimi?” 7 Kwa
hiyo akamjibu mfalme, “Kwa mtu
ambaye mfalme apenda kumheshimu,
8 [c]aletewe joho la kifalme ambalo mfalme
ameshalivaa na farasi ambaye mfalme
alishampanda, ambaye amevikwa taji ya
kifalme kichwani mwake. 9 [d]Kisha joho na
farasi vikabidhiwe kwa mmojawapo wa
wakuu wa mfalme anayeheshimika sana.
Nao wamvike mtu yule ambaye mfalme
anapenda kumheshimu, na aongozwe
akiwa juu ya farasi kupitia barabara za
mji, wakitangaza mbele yake, ‘Hivi ndivyo
anavyofanyiwa mtu ambaye mfalme apenda
kumheshimu!’ ”

10 Mfalme akamwamuru Hamani, “Nenda
mara moja, chukua joho na farasi na
ufanye kama vile ulivyopendekeza kwa
Mordekai Myahudi, akaaye langoni mwa
mfalme. Usipuuze kufanya kitu chochote
ulichoshauri.”

11 Hivyo Hamani akachukua joho na
farasi.

Akamvika Mordekai, na kumpandisha juu
ya farasi akamtembeza katika barabara za
mji akitangaza mbele yake, “Hivi ndivyo
anavyofanyiwa mtu ambaye mfalme
anapenda kumheshimu!”

12 [e]Baadaye Mordekai akarudi kwenye
lango la mfalme. Lakini Hamani akakimbia
nyumbani, akiwa amejaa huzuni, 13 [f]naye
akamweleza Zereshi mkewe pamoja
na rafiki zake wote kila kitu ambacho
kimempata.

Washauri wake pamoja na Zereshi
mkewe wakamwambia, “Kwa kuwa
Mordekai, ambaye mbele yake umeanza
kuanguka ni wa asili ya Kiyahudi, huwezi
kushindana naye; kwa hakika utaanguka!”
14 Walipokuwa bado wakizungumza
naye, matowashi wa mfalme wakaja na
kumharakisha Hamani aende katika karamu
aliyoiandaa Esta.

*Hamani Aangikwa*

7 [g]Basi mfalme na Hamani wakaenda
kula chakula pamoja na Malkia Esta.
2 [h]Walipokuwa wakinywa mvinyo katika
siku ya pili, mfalme akauliza tena, “Malkia
Esta, ni nini haja yako? Utapewa. Ombi lako
ni nini? Hata nusu ya ufalme, utapewa.”

3 Kisha Malkia Esta akajibu, “Kama
nimepata kibali kwako, ee mfalme, tena
kama inapendeza utukufu wako, nijalie
maisha yangu, hii ndiyo haja yangu.
Pia uokoe watu wangu, hili ndilo ombi
langu. 4 [i]Kwa kuwa mimi na watu wangu
tumeuzwa kwa kuangamizwa, kuchinjwa na
kuharibiwa. Kama tungalikuwa tumeuzwa
tu kuwa watumwa wa kiume na wa kike,
ningalinyamaza kimya, kwa sababu

[a]**6:1** Dan 6:18; Es 2:23
[b]**6:3** Mhu 9:13-16
[c]**6:8** Mwa 41:42; Isa 52:1
[d]**6:9** Mwa 41:43
[e]**6:12** 2Sam 15:30; Mik 3:7
[f]**6:13** Za 57:6; Mit 26:27
[g]**7:1** Mwa 40:20-21; Mt 22:1-14
[h]**7:2** Es 5:3
[i]**7:4** Es 3:9

shida kama hii isingalitosha kumsumbua
mfalme."
5 Mfalme Ahasuero akamuuliza Malkia
Esta, "Ni nani huyu? Yuko wapi mtu huyu
aliyethubutu kufanya jambo kama hili?"
6 Esta akasema, "Mtesi na adui ni huyu
mwovu Hamani."

Hamani alifadhaika mbele ya mfalme na
malkia. 7 [a]Mfalme akainuka kwa ghadhabu,
akaacha mvinyo wake, akaenda kwenye
bustani ya jumba la kifalme. Lakini Hamani,
akitambua kwamba mfalme ameshaamua
hatima yake, alibaki nyuma kumsihi Malkia
Esta aokoe maisha yake.
8 Mara mfalme aliporudi kutoka bustani
ya jumba la kifalme na kuja kwenye ukumbi
wa karamu, Hamani alikuwa akijitupa
juu ya kiti mahali ambapo Esta alikuwa
akiegemea.

Mfalme akasema kwa nguvu, "Je,
atamdhalilisha malkia hata huku nyumbani
akiwa pamoja nami!"

Mara neno lilipotoka kinywani mwa
mfalme, walifunika uso wa Hamani.
9 [b]Kisha Harbona, mmoja wa matowashi
wanaomtumikia mfalme, akasema, "Mahali
pa kuangika watu penye urefu wa mita
ishirini na mbili pako nyumbani mwa
Hamani. Alikuwa amepatengeneza kwa
ajili ya Mordekai, ambaye alizungumza ili
kumsaidia mfalme."

Mfalme akasema, "Mwangikeni juu
yake!" 10 [c]Kwa hiyo wakamtundika Hamani
mahali alipokuwa ameandaa kwa ajili ya
Mordekai. Ndipo ghadhabu ya mfalme
ikatulia.

*Amri Ya Mfalme Kuhusu Wayahudi*

8 [d]Siku ile ile Mfalme Ahasuero akampa
Malkia Esta shamba la Hamani, adui wa
Wayahudi. Naye Mordekai akaja mbele ya
mfalme, kwa kuwa Esta alikuwa amesema
jinsi anavyohusiana naye. 2 [e]Mfalme
akaivua pete yake ya muhuri, ambayo
alikuwa amemnyang'anya Hamani, akampa
Mordekai, naye Esta akamweka Mordekai
juu ya shamba la Hamani.
3 [f]Esta alimsihi tena mfalme, akianguka
miguuni pake na kulia. Akamwomba
akomeshe mpango mwovu wa Hamani
Mwagagi ambao alikuwa ameupanga dhidi
ya Wayahudi. 4 [g]Kisha mfalme alimnyooshea
Esta fimbo yake ya utawala ya dhahabu
naye aliinuka na kusimama mbele yake.
5 Esta akasema, "Kama ikimpendeza
mfalme, nami kama nikipata kibali naye
akiona ni jambo lililo sawa kunitendea na
kama akipendezwa nami, basi iandikwe
amri ya kuzitangua barua zile Hamani
mwana wa Hamedatha, Mwagagi,
alizotunga na kuandika kuangamiza
Wayahudi katika majimbo yote ya mfalme.
6 Kwa maana nitawezaje kuvumilia kuona
maafa yakiwapata watu wangu? Nitawezaje
kuvumilia kuona maangamizi ya jamaa
yangu?"
7 Mfalme Ahasuero akawajibu Malkia
Esta na Mordekai Myahudi, "Kwa sababu
Hamani aliwashambulia Wayahudi,
nimetoa shamba la Hamani kwa Esta, naye
ameangikwa kwenye mti wa kunyongea.
8 [h]Basi andika amri nyingine kwa jina
la mfalme kwa ajili ya Wayahudi kama
unavyoona vyema, kisha uifunge kwa kutia
muhuri kwa pete ya mfalme kwa kuwa
hakuna andiko lililoandikwa kwa jina la
mfalme na kutiwa muhuri kwa pete ya
mfalme linaloweza kutanguliwa."
9 [i]Mara moja waandishi wa mfalme
wakaitwa kwenye siku ya ishirini na tatu,
mwezi wa tatu, ndio mwezi wa Siwani.
Wakaandika yote Mordekai aliyoamuru
kwa Wayahudi, kwa majemadari, watawala
na wakuu wa majimbo 127 kuanzia
Bara Hindi mpaka Kushi.[j] Maagizo haya
yaliandikwa kwa maandishi ya kila jimbo
na kwa lugha ya kila mtu pia kwa Wayahudi
kwa maandishi yao wenyewe na lugha yao.
10 Mordekai aliandika nyaraka kwa jina la
Mfalme Ahasuero, akazitia muhuri kwa

[a]**7:7** Mwa 34:7; 2Fal 21:18
[b]**7:9** Za 7:14-16; Mit 11:5-6
[c]**7:10** Mwa 40:22; Mit 10:28
[d]**8:1** Mit 22:22-23
[e]**8:2** Mwa 24:22; Dan 2:48
[f]**8:3** Kut 17:8-16
[g]**8:4** Es 4:11
[h]**8:8** Es 1:19; Mwa 41:42
[i]**8:9** Es 1:1; Neh 13:24
[j]9 Kushi hapa ina maana ya Ethiopia.

pete ya mfalme na kuzipeleka kwa njia ya matarishi, ambao waliendesha farasi waendao kasi waliozalishwa maalum kwa ajili ya mfalme.

11 Waraka wa mfalme uliwaruhusu Wayahudi katika kila mji kuwa na haki ya kukusanyika na kujilinda wenyewe; kuharibu, kuua na kuangamiza jeshi lolote, taifa lolote au jimbo lile litakalowashambulia wao, wake zao, watoto wao na kuteka mali za adui zao. 12 Siku ambayo iliwekwa kwa Wayahudi kufanya hili katika majimbo yote ya Mfalme Ahasuero ilikuwa siku ya kumi na tatu ya mwezi wa kumi na mbili, yaani mwezi wa Adari. 13 [a]Nakala ya tangazo ilikuwa itolewe kama sheria katika kila jimbo na iweze kujulikana kwa watu wa kila taifa, ili kwamba Wayahudi wawe tayari siku hiyo kulipiza kisasi kwa adui zao.

14 Matarishi, wakiwa wamepanda farasi wa kifalme, walitoka mbio wakichochewa na agizo la mfalme. Tangazo lilitolewa pia katika ngome ya mji wa Shushani.

15 [b]Mordekai akaondoka mbele ya mfalme akiwa amevaa mavazi ya kifalme ya buluu na nyeupe, taji kubwa la dhahabu na joho la zambarau la kitani safi. Na mji wa Shushani ukasherehekea kwa furaha. 16 [c]Kwa maana kwa Wayahudi ulikuwa wakati wa raha na furaha, shangwe na heshima. 17 [d]Katika kila jimbo na katika kila jiji, popote waraka wa mfalme ulipofika, kulikuwepo furaha na shangwe miongoni mwa Wayahudi, pamoja na karamu na kushangilia. Na watu wengi wa mataifa mengine wakajifanya Wayahudi kwa sababu ya kuwahofu Wayahudi.

### *Ushindi Wa Wayahudi*

9 [e]Katika siku ya kumi na tatu ya mwezi wa kumi na mbili, yaani mwezi wa Adari, amri iliyoagizwa na mfalme ilikuwa itekelezwe. Siku hii adui wa Wayahudi walikuwa wametumaini kuwashinda, lakini sasa mambo yaliwageukia na Wayahudi wakawashinda wale waliokuwa wanawachukia. 2 [f]Wayahudi walikusanyika katika miji yao, katika majimbo ya Mfalme Ahasuero kuwashambulia wale waliokuwa wanatafuta kuwaangamiza. Hakuna yeyote aliyeweza kushindana nao, kwa sababu watu wa mataifa mengine yote waliwaogopa. 3 Nao wakuu wote wa majimbo, majemadari, watawala na maafisa wa mfalme wakawasaidia Wayahudi, kwa sababu walimhofu Mordekai. 4 [g]Mordekai alikuwa mtu mashuhuri katika jumba la mfalme; sifa zake zilienea katika majimbo yote naye alipata uwezo zaidi na zaidi.

5 [h]Wayahudi waliwaangusha adui zao wote kwa upanga wakiwaua na kuwaangamiza, nao walifanya kile walichotaka kwa wale waliowachukia. 6 Katika ngome ya Shushani Wayahudi waliua na kuangamiza wanaume 500. 7 Pia waliwaua Parshendatha, Dalfoni, Aspatha, 8 Poratha, Adalia, Ardatha, 9 Parmashta, Arisai, Aridai na Waizatha, 10 [i]wana kumi wa Hamani mwana wa Hamedatha, adui wa Wayahudi. Lakini hawakuchukua nyara.

11 Mfalme aliarifiwa siku iyo hiyo hesabu ya waliouawa katika ngome ya Shushani. 12 [j]Mfalme akamwambia Malkia Esta, "Wayahudi wamewaua wanaume 500 na wana kumi wa Hamani ndani ya ngome ya Shushani. Wamefanyaje katika majimbo mengine ya mfalme yaliyobaki? Je, sasa haja yako ni nini? Nayo pia utapewa. Nalo ombi lako ni nini? Nalo utafanyiwa."

13 Esta akajibu, "Ikimpendeza mfalme, uwape ruhusa Wayahudi walioko Shushani warudie amri ya leo kesho pia, na wana wa Hamani kumi wanyongwe mahali pa kunyongea watu."

14 [k]Basi mfalme akaamuru kwamba hili litendeke. Amri ilitolewa huko Shushani, nao wakawanyonga wana kumi wa Hamani. 15 [l]Wayahudi huko Shushani wakakusanyika

[a] **8:13** Es 1:1; Neh 13:24
[b] **8:15** 2Sam 12:30; Mwa 41:42
[c] **8:16** Za 112:4; Yer 29:4-7
[d] **8:17** Za 35:27; Kum 11:25
[e] **9:1** Yer 29:4-7; Mit 22:22-23
[f] **9:2** Mwa 22:17; Za 35:26
[g] **9:4** Kum 25:17-19; Ezr 4:6
[h] **9:5** Kum 25:17-19; Ezr 4:6
[i] **9:10** Es 5:11; Mwa 14:23
[j] **9:12** Es 5:6; 7:2
[k] **9:14** Ezr 6:11
[l] **9:15** Mwa 14:23

pamoja siku ya kumi na nne ya mwezi wa
Adari, nao wakawaua wanaume 300 huko
Shushani, lakini hawakuchukua nyara zao.
16 [a]Wakati ule ule, Wayahudi wengine
waliokuwa kwenye majimbo ya mfalme,
wakakusanyika kujilinda nao wakapata
nafuu kutokana na adui zao. Waliua adui
zao wapatao 75,000 lakini hawakugusa
nyara zao. 17 [b]Hili lilitendeka siku ya kumi
na tatu ya mwezi wa Adari na siku ya kumi
na nne walipumzika na kuifanya siku ya
karamu na furaha.

*Kusherehekea Purimu*

18 Wayahudi huko Shushani, hata hivyo,
walikuwa wamekusanyika siku ya kumi na
tatu na ya kumi na nne, pia siku ya kumi
na tano walipumzika na kuifanya siku ya
karamu na furaha.
19 [c]Ndiyo sababu Wayahudi wanaokaa
vijijini na katika miji midogo huadhimisha
siku ya kumi na nne ya mwezi wa Adari
kama siku ya furaha na karamu, siku
ambayo wao hupeana zawadi mmoja kwa
mwingine.
20 Mordekai aliandika matukio haya,
naye akapeleka barua kwa Wayahudi
wote walioko katika majimbo ya Mfalme
Ahasuero, majimbo yaliyo mbali na karibu,
21 akiwataka kila mwaka washerehekee siku
ya kumi na nne na ya kumi na tano ya
mwezi wa Adari 22 [d]kama wakati ambao
Wayahudi walipata nafuu kutoka kwa adui
zao na kama mwezi ambao huzuni yao
iligeuzwa kuwa furaha na kuomboleza kwao
kuwa siku ya kusherehekea. Aliwaandikia
kushika siku hizo kama siku za karamu na
za furaha na kupeana zawadi za vyakula
wao kwa wao na zawadi kwa maskini.
23 Hivyo Wayahudi walikubali kuendeleza
sherehe walizokuwa wamezianza,
wakifanya lile Mordekai alilokuwa
amewaandikia. 24 [e]Kwa maana Hamani
mwana wa Hamedatha Mwagagi, adui wa
Wayahudi wote, alikuwa amepanga hila
dhidi ya Wayahudi ili kuwaangamiza,
na alikuwa amepiga *puri* (yaani kura)
kwa ajili ya maangamizi na uharibifu
wao. 25 [f]Lakini wakati shauri hilo baya
lilipoarifiwa kwa mfalme, alitoa amri
iliyoandikwa kwamba mipango mibaya
ambayo Hamani ameipanga dhidi ya
Wayahudi inapasa imrudie juu ya kichwa
chake mwenyewe, na kwamba yeye na
wanawe waangikwe mahali pa kunyongea
watu. 26 (Kwa hiyo siku hizi ziliitwa Purimu,
kutokana na neno *puri.*) Kwa sababu ya kila
kitu kilichoandikwa kwenye barua hii na
kwa sababu ya yale waliyoyaona na yale
yaliyowatokea, 27 Wayahudi wakachukua
na kuifanya desturi kwamba wao na
wazao wao na wote ambao walijiunga nao
wangefanya bila kuacha kushika siku hizi
mbili kila mwaka, kwa njia ilivyoelekezwa
na kwa wakati wake. 28 Siku hizi zinapasa
zikumbukwe na kuadhimishwa katika kila
kizazi, kila jamaa na katika kila jimbo na
kila jiji. Nazo siku hizi za Purimu kamwe
zisikome kusherehekewa na Wayahudi,
wala kumbukumbu zake zisipotee miongoni
mwa wazao wake.
29 Basi Malkia Esta binti Abihaili, pamoja
na Mordekai, Myahudi, waliandika kwa
mamlaka yote kuthibitisha barua hii ya
pili kuhusu Purimu. 30 [g]Naye Mordekai
akatuma barua kwa Wayahudi wote
katika majimbo 127 ya ufalme wa
Ahasuero, barua zenye maneno ya amani
na matumaini, 31 [h]ili kuimarisha siku hizi
za Purimu katika majira yake yaliyowekwa,
kama Mordekai, Myahudi na Malkia Esta
walivyowaamuru, na walivyojiimarisha
wenyewe na wazao wao kuhusu nyakati
za kufunga na kuomboleza. 32 Amri ya Esta
ilithibitisha taratibu hizi kuhusu Purimu,
nayo ikaandikwa katika kumbukumbu.

*Ukuu Wa Mordekai*

10 [i]Mfalme Ahasuero alitoza ushuru
katika ufalme wake wote hadi kwenye

[a]**9:16** Kum 25:19; 1Nya 4:43
[b]**9:17** 1Fal 3:15
[c]**9:19** Ufu 11:10
[d]**9:22** Neh 8:12; Za 30:11-12
[e]**9:24** Kut 17:8-16; Law 16:8
[f]**9:25** Za 7:16; Es 7:10
[g]**9:30** Es 1:1
[h]**9:31** Es 4:1-3
[i]**10:1** Za 72:10; 97:1

miambao yake ya mbali. 2 [a]Matendo yake
yote ya nguvu na uwezo, pamoja na habari
zote za ukuu wa Mordekai ambao mfalme
alikuwa amemkuza, je, hayakuandikwa
katika kitabu cha kumbukumbu za wafalme
wa Umedi na Uajemi? 3 [b]Mordekai Myahudi
alikuwa wa pili kwa cheo kutoka Mfalme
Ahasuero, naye alikuwa bora kabisa
miongoni mwa Wayahudi, akipandishwa
katika heshima ya juu na ndugu zake
Wayahudi kwa sababu aliwatendea mema
watu wake, na alizungumza kwa ajili ya
ustawi wa Wayahudi wote.

---

[a]**10:2** Es 8:15; Mwa 41:44
[b]**10:3** Dan 5:7; Mwa 41:40; Neh 2:10

# AYUBU

## SEHEMU YA KWANZA: HABARI ZA AWALI

*(Ayubu 1–2)*

*Ayubu Na Jamaa Yake*

1 [a]Katika nchi ya Usi paliishi mtu ambaye
aliitwa Ayubu. Mtu huyu alikuwa hana
hatia, naye alikuwa mkamilifu; alimcha
Mungu na kuepukana na uovu. 2 [b]Alikuwa
na wana saba na binti watatu, 3 [c]naye
alikuwa na kondoo elfu saba, ngamia elfu
tatu, jozi mia tano za maksai, na punda
mia tano, tena alikuwa na idadi kubwa
ya watumishi. Alikuwa mtu mkuu sana
miongoni mwa watu wa Mashariki.
4 [d]Wanawe walikuwa na desturi ya
kufanya karamu katika nyumba zao kwa
zamu, nao wangewaalika umbu zao watatu
ili kula na kunywa pamoja nao. 5 [e]Wakati
kipindi cha karamu kilimalizika, Ayubu
angetuma waitwe na kuwafanyia utakaso.
Angetoa dhabihu ya sadaka ya kuteketezwa
kwa ajili ya kila mmoja wao asubuhi na
mapema, akifikiri, "Pengine wanangu
wametenda dhambi na kumlaani Mungu
mioyoni mwao." Hii ilikuwa ndiyo desturi
ya kawaida ya Ayubu.

*Jaribu La Kwanza La Ayubu*

6 [f]Siku moja wana wa Mungu[g] walikwenda
kujionyesha mbele za BWANA. Shetani[h] naye
akaja pamoja nao. 7 [i]BWANA akamwambia
Shetani, "Umetoka wapi?"
Shetani akamjibu BWANA, "Natoka
kuzunguka pote duniani, nikitembea huku
na huko humo."
8 [j]Ndipo BWANA akamwambia Shetani,
"Je, umemwangalia huyo mtumishi wangu
Ayubu? Hakuna mtu mwingine duniani
aliye kama yeye, asiye na hatia, ni mnyofu,
mwenye kumcha Mungu, na kuepukana na
uovu."
9 [k]Shetani akamjibu BWANA, "Je, Ayubu
anamcha Mungu bure? 10 [l]Je, wewe
hukumjengea boma pande zote yeye na wa
nyumbani mwake pamoja na kila kitu alicho
nacho? Kazi za mikono yake umezibariki na
hivyo makundi yake ya kondoo na mbuzi
pamoja na ya wanyama yameenea katika
nchi nzima. 11 [m]Lakini nyoosha mkono wako
na kupiga kila kitu alicho nacho, naye kwa
hakika atakulaani mbele za uso wako."
12 [n]BWANA akamwambia Shetani, "Vema
sana, kwa hiyo, kila kitu alicho nacho kiko
mikononi mwako, lakini juu ya huyo mtu
mwenyewe usimguse hata kwa kidole."
Ndipo Shetani akatoka mbele za BWANA.
13 [o]Siku moja watoto wa Ayubu
walipokuwa wakifanya karamu wakila na
kunywa divai katika nyumba ya ndugu yao
mkubwa, 14 [p]akaja mjumbe kwa Ayubu na
kusema, "Maksai walikuwa wakilima na
punda walikuwa wakilisha karibu nao,

---

[a]**1:1** Mwa 22:21; Yak 5:11; Eze 14:14, 20; Mit 8:13; Mwa 10:23; 6:9; 22:12; Ay 23:7, 10; 2:3; Za 11:7; 107:42; Mit 21:29; Mik 7:2; Kum 4:6; 1The 5:22

[b]**1:2** Za 127:3; Rut 4:15; Ay 1:13, 18; 42:13; Za 144:12

[c]**1:3** Ay 29:25; Mwa 13:2; 12:16; Ay 1:8; Mwa 25:6; Ay 42:10; Za 103:10

[d]**1:4** Ay 1:13, 18

[e]**1:5** Mwa 8:20; Ay 42:8; 1Fal 21:10-13; Za 74:10; Neh 12:30; Ay 8:4; Za 10:3

[f]**1:6** 1Fal 22:19; Ay 38:7; 2:1; Dan 7:10; Mwa 6:2; 2Sam 24:1; 2Nya 18:21; Za 109:6; Lk 22:31

[g]6 Wana wa Mungu hapa ina maana malaika au viumbe vya mbinguni.

[h]6 Shetani hapa ina maana ya mshtaki wa watakatifu.

[i]**1:7** Mwa 3:1; 1Pet 5:8; Mt 12:43

[j]**1:8** Ay 42:7-8; Kut 20:20; Yos 1:7; Za 25:16; 26:12; 112:1; 128:4

[k]**1:9** 1Tim 6:5

[l]**1:10** Za 34:7; 128:1-2; Ay 8:7; 1Sam 25:16; Ay 2:4; 29:6; 42:12, 17

[m]**1:11** Ay 19:21; Law 24:11; Ufu 12:9-10; Lk 22:31; Isa 3:8; 65:3; Ay 2:5

[n]**1:12** Ay 2:6; 1Kor 10:13

[o]**1:13** Ay 1:2, 4; Mhu 9:12; Lk 12:19, 20

[p]**1:14** Mwa 36:24

15 [a]Waseba wakawashambulia na kuchukua mifugo. Kisha wakawaua watumishi kwa upanga, nami ndimi peke yangu niliyenusurika kukuletea habari!"
16 [b]Alipokuwa bado ananena, mjumbe mwingine akaja na kusema, "Moto wa Mungu ulishuka kutoka mbinguni na kuteketeza kondoo na watumishi, nami ndimi peke yangu niliyenusurika kukuletea habari!"
17 [c]Alipokuwa bado ananena, mjumbe mwingine akaja na kusema, "Wakaldayo waliunda vikosi vitatu vya uvamizi na kuwaangukia ngamia wako na kuwachukua wakaondoka nao. Wakawaua watumishi kwa upanga, nami ndimi peke yangu niliyenusurika kukuletea habari."
18 [d]Alipokuwa bado ananena, mjumbe mwingine akaja na kusema, "Wana wako na binti zako walipokuwa wakifanya karamu, wakila na kunywa divai katika nyumba
ya ndugu yao mkubwa, 19 [e]ghafula upepo
wenye nguvu ukavuma kutoka jangwani, nao ukaipiga nyumba hiyo pembe zake nne. Ikawaangukia hao watoto nao wamekufa, nami ndimi peke yangu niliyenusurika kukuletea habari!"
20 [f]Ndipo Ayubu akasimama, akararua joho lake na kunyoa nywele zake. Kisha
akaanguka chini katika kuabudu 21 [g]na
kusema:

"Nilitoka tumboni mwa mama yangu
uchi,
nami nitaondoka uchi,[h]
Bwana alinipa, naye Bwana
ameviondoa,
jina la Bwana litukuzwe."

22 [i]Katika mambo haya yote, Ayubu hakutenda dhambi kwa kumlaumu Mungu kwa kufanya ubaya.

### *Jaribu La Pili La Ayubu*

2 [j]Siku nyingine wana wa Mungu walikuja kujionyesha mbele za Bwana. Shetani naye akaja pamoja nao kujionyesha mbele
zake. 2 [k]Bwana akamuuliza Shetani,
"Umetoka wapi?"
Shetani akamjibu Bwana "Natoka kuzunguka pote duniani, nikitembea huku na huko humo."
3 [l]Bwana akamwambia Shetani, "Je, umemwangalia huyo mtumishi wangu Ayubu? Hakuna mtu mwingine duniani aliye kama yeye, mtu asiye na hatia, ni mnyofu, mwenye kumcha Mungu na kuepukana na uovu. Naye bado anadumisha uadilifu wake, ingawa ulinichochea dhidi yake, ili nimwangamize pasipo sababu."
4 [m]Shetani akamjibu Bwana, "Ngozi kwa ngozi! Mwanadamu atatoa vyote alivyo
navyo kwa ajili ya uhai wake. 5 [n]Lakini
nyoosha mkono wako na kuipiga nyama yake na mifupa yake, naye kwa hakika atakulaani mbele za uso wako."
6 [o]Bwana akamwambia Shetani, "Vema sana, kwa hiyo, yeye yumo mikononi mwako, lakini lazima umwachie uhai wake."
7 [p]Basi Shetani akatoka mbele za Bwana naye akampiga Ayubu kwa majipu mabaya tangu nyayo za miguu yake hadi utosi wa

[a]**1:15** Mwa 10:7; Ay 6:19; 9:26
[b]**1:16** 1Fal 18:38; 2Fal 1:12; Ay 20:26; Mwa 18:17; Law 10:2; Hes 11:1-3
[c]**1:17** Mwa 11:28-31; Ay 9:24
[d]**1:18** Ay 1:2, 4
[e]**1:19** Isa 21:1; Mk 7:25; Za 11:6; Isa 5:28; Yer 4:11; 13:24; 18:17; Eze 17:10; Hos 13:15
[f]**1:20** Mwa 37:29; Mk 14:63; Isa 3:24; 15:2; 22:12; Yer 7:29; 16:6; Eze 27:31; 29:18; Mik 1:16; 1Pet 5:6
[g]**1:21** Mhu 5:15; Rut 1:21; Amu 10:15; Efe 5:20; Mwa 45:5; 1Tim 6:7; 1Sam 2:7; Mhu 7:14; Yak 5:11; Amo 3:6; Efe 5:20; Mwa 45:5
[h]21 Au: nitarudi huko uchi.
[i]**1:22** Mit 10:19; Rum 9:20; Ay 2:10; Za 39:1; Isa 53:7
[j]**2:1** Ay 1:6; Mwa 6:2
[k]**2:2** Mwa 3:1
[l]**2:3** Kut 20:20; Ay 6:29; 9:17; 13:18; Yak 1:12; Za 44:17; Ay 13:18; 27:5, 6; 1Pet 1:7; Mt 7:11; Yn 9:2
[m]**2:4** Ay 1:10
[n]**2:5** Za 102:5; Ay 19:20; Mao 4:8; Za 32:3, 4; Ay 16:8; 1:11
[o]**2:6** Ay 1:12; 2Kor 12:7
[p]**2:7** Kum 28:35; Ay 7:5; 16:16

kichwa. [8] [a]Ndipo Ayubu akachukua kigae na kujikuna nacho huku akiketi kwenye majivu.

[9] [b]Mke wake akamwambia, “Je, bado unashikamana na uadilifu wako? Mlaani Mungu nawe ukafe!”

[10] [c]Akamjibu, “Unazungumza kama vile ambavyo mwanamke mpumbavu[d] yeyote angenena. Je, tupokee mema mikononi mwa Mungu, nasi tusipokee na udhia?”

Katika mambo haya yote, Ayubu hakutenda dhambi katika kusema kwake.

### *Marafiki Watatu Wa Ayubu*

[11] [e]Basi marafiki watatu wa Ayubu,
ndio Elifazi Mtemani, na Bildadi Mshuhi
na Sofari Mnaamathi, waliposikia juu ya
taabu yote iliyompata Ayubu, wakajipanga
toka manyumbani mwao, nao wakakutana
pamoja kwa makubaliano kwenda
kumtuliza katika taabu hiyo na kumfariji.
[12] [f]Walipomwona kwa mbali, ilikuwa
vigumu kumtambua. Wakaanza kulia kwa
sauti kubwa, wakayararua majoho yao na
kujirushia mavumbi juu ya vichwa vyao.
[13] [g]Kisha wakaketi chini kwenye udongo
pamoja na Ayubu kwa siku saba usiku na
mchana. Hakuna yeyote aliyesema naye
neno, kwa sababu waliona jinsi mateso yake
yalivyokuwa makubwa.

[a]**2:8** 2Sam 13:19; Za 7:5; Mt 11:21; Mwa 18:27; Es 4:3; Ay 16:15; 19:9; 42:6; Isa 5:8; 6:13; Yer 6:26; Mao 3:29; Eze 26:16; Yon 3:5-8

[b]**2:9** Ay 1:21; 13:15; 27:5; 33:9; 35:2; 1The 5:8; Kut 20:7; 2Fal 6:33

[c]**2:10** Mhu 2:24; Mao 3:38-41; Yak 5:11; Za 39:1

[d]10 Mpumbavu hapa ina maana ya kupungukiwa maadili.

[e]**2:11** Mwa 25:2; 36:11; 37:35; Yer 49:7; Rum 12:15; Ay 11:1; 20:1; Yn 11:19

[f]**2:12** 2Sam 1:2; Neh 9:1; Eze 27:30; Ay 17:7; Isa 52:14; Mwa 37:29; Mk 14:63; Yos 7:6

[g]**2:13** Mwa 50:10-12; Eze 3:15; Isa 3:26; 47:1; Eze 26:16; Yn 3:6; Hag 2:22; Mit 17:28; Isa 23:2; 47:5

## SEHEMU YA PILI: MAZUNGUMZO YA AYUBU NA RAFIKI ZAKE WATATU

*(Ayubu 3–31)*

### HOTUBA YA KWANZA YA AYUBU

### *Ayubu Anazungumza*

[1] [h]Baada ya jambo hili, Ayubu akafumbua
kinywa chake na kuilaani siku ya kuzaliwa
kwake.
[2] Kisha akasema:

[3] [i]“Siku ya kuzaliwa kwangu na
ipotelee mbali,
nao usiku ule iliposemekana,
‘Mtoto wa kiume amezaliwa!’
[4] Siku ile na iwe giza;
Mungu juu na asiiangalie;
nayo nuru isiiangazie.
[5] [j]Giza na kivuli kikuu kiikalie tena;
wingu na likae juu yake;
weusi na uifunike nuru yake.
[6] [k]Usiku ule na ushikwe na giza kuu;
usihesabiwe katika siku za mwaka,
wala usihesabiwe katika siku za
mwezi wowote.
[7] [l]Usiku ule na uwe tasa;
sauti ya furaha na isisikike ndani
yake.
[8] [m]Wale wazilaanio siku wailaani hiyo
siku,
wale walio tayari kumwamsha
Lewiathani.[n]
[9] [o]Nyota zake za alfajiri na ziwe giza;
nao ungojee mwanga bila
mafanikio,
wala usiuone mwonzi wa kwanza
wa mapambazuko,

[h]**3:1** Yer 15:10; 20:14

[i]**3:3** Mhu 6:3; Ay 10:18-19; Yer 15:10; Ay 3:11, 16; Mit 26:24

[j]**3:5** Za 44:19; Yer 13:16; Ay 16:16; Isa 9:2; Za 23:4; Mt 4:16; Lk 1:79; Mhu 4:2

[k]**3:6** Ay 23:17; 30:26; Za 20:5; 33:3; 65:13; Isa 26:19

[l]**3:7** Za 20:5; 33:3; Isa 26:19; Yer 51:48

[m]**3:8** Yer 9:17

[n]8 Lewiathani ni mnyama mkubwa wa baharini mwenye magamba anayefanana na joka kubwa, mwenye umbo la kutisha, asiyeweza kuvuliwa.

[o]**3:9** Ay 41:18; Hab 3:4

10 kwa sababu huo usiku haukunifungia
mlango wa tumbo la mama yangu,
ili kuyaficha macho yangu
kutokana na taabu.

11 [a]"Kwa nini sikuangamia wakati wa
kuzaliwa?
Kwa nini sikufa nilipokuwa
ninatoka tumboni?
12 [b]Kwa nini pakawa na magoti ya
kunipokea
na matiti ili nipate
kunyonyeshwa?
13 [c]Kwa maana sasa ningekuwa
nimepumzika kwa amani.
Ningekuwa nimelala na
kupumzika
14 [d]pamoja na wafalme na washauri wa
dunia,
waliojijengea mahali ambapo sasa
ni magofu,
15 [e]pamoja na watawala waliokuwa na
dhahabu,
waliozijaza nyumba zao kwa
fedha.
16 [f]Au kwa nini sikufichwa ardhini
kama mtoto aliyezaliwa mfu,
kama mtoto mchanga ambaye
kamwe hakuuona mwanga?
17 [g]Huko waovu huacha kusumbua
na huko waliochoka hupumzika.
18 [h]Wafungwa nao hufurahia utulivu
wao,
hawasikii tena sauti ya kukemea
ya kiongozi wa watumwa.
19 [i]Wadogo na wakubwa wamo humo,
na mtumwa ameachiwa huru
kutoka kwa bwana wake.

20 [j]"Mbona nuru inawaangazia wale
walio taabuni,
na hao wenye uchungu kupewa
uhai,
21 [k]wale wanaotamani kifo ambacho
hakiji,
wale watafutao kufa zaidi ya
kutafuta hazina iliyofichwa,
22 [l]ambao hujawa na furaha,
na hushangilia wafikapo kaburini?
23 [m]Kwa nini uhai hupewa mtu
ambaye njia yake imefichika,
ambaye Mungu amemzungushia
boma?
24 [n]Kwa maana kulia kwangu kwa
uchungu kwanijia badala ya
chakula;
kusononeka kwangu kunamwagika
kama maji.
25 [o]Lile nililokuwa naliogopa limenijia;
lile nililokuwa ninalihofia
limenipata.
26 [p]Sina amani, wala utulivu;
sina pumziko, bali taabu tu."

*Elifazi Anazungumza: Ayubu Ametenda Dhambi*

4 [q]Ndipo Elifazi Mtemani akajibu:

2 [r]"Kama mtu
akithubutu kuzungumza
nawe,
kutakukasirisha?

[a]**3:11** Ay 3:3
[b]**3:12** Mwa 30:3; 48:12; Isa 66:12
[c]**3:13** Ay 17:13; 30:23; 3:17; 7:8-10, 21; 3:19; 14:10-12; Za 139:11; Isa 8:22
[d]**3:14** Isa 14:9; Eze 32:28-32; Yer 51:37; Nah 3:7; Ay 9:24; 12:17; 15:28
[e]**3:15** Ay 12:21; 15:29; 20:10; 27:17; Mit 13:22; Sef 1:11; Isa 45:1; Za 49:16-17; 45:1; Mit 13:22
[f]**3:16** Mhu 6:3; 4:3; Za 58:8; 71:6
[g]**3:17** Ay 3:26; 30:26; 17:16; Mhu 4:2; Isa 14:3
[h]**3:18** Ay 38:7; 39:7; Isa 51:14; Mwa 15:13
[i]**3:19** Ay 9:22; 17:16; 21:33; 24:24; 30:23; Mhu 12:5
[j]**3:20** Yer 20:18; Eze 27:30-31; 1Sam 1:10
[k]**3:21** Ufu 9:6; Mit 2:4; Za 119:127
[l]**3:22** Ay 7:16; Mhu 4:3; Yer 8:3
[m]**3:23** Mao 2:4; 3:7; Hos 2:6; Mt 4:19; Isa 59:10; Yer 13:16; 23:12; Ay 6:4; 16:13; Za 88:8
[n]**3:24** Ay 33:20; Mao 2:12; 1Sam 1:15; Isa 35:10; 53:12; Za 6:6; 22:1; 32:3; 107:18
[o]**3:25** Hos 13:3; Ay 7:9; 30:15; 9:28; Mwa 42:36
[p]**3:26** Dan 4:5; Mt 11:28; Isa 48:22; Yn 14:27
[q]**4:1** Mwa 36:11; Ay 15:1; 22:1
[r]**4:2** Yer 4:19; 20:9; Ay 32:20

Lakini ni nani awezaye
kujizuia asiseme?
3 [a]Fikiri jinsi ambavyo umewafundisha
watu wengi,
jinsi ambavyo umeitia nguvu
mikono iliyokuwa dhaifu.
4 [b]Maneno yako yamewategemeza
wale waliojikwaa;
umeyatia nguvu magoti
yaliyokuwa dhaifu.
5 [c]Lakini sasa hii taabu imekujia
wewe,
nawe unashuka moyo;
imekupiga wewe,
nawe unafadhaika.
6 [d]Je, kumcha Mungu kwako
hakupaswi kuwa
ndiyo matumaini yako
na njia zako kutokuwa na lawama
ndilo taraja lako?

7 [e]"Fikiri sasa: Ni mtu yupi asiye
na hatia ambaye aliwahi
kuangamia?
Ni wapi wanyofu waliwahi
kuangamizwa?
8 [f]Kwa jinsi ambavyo mimi
nimechunguza,
wale walimao ubaya
na wale hupanda uovu,
huvuna hayo hayo hayo.
9 [g]Kwa pumzi ya Mungu
huangamizwa;
kwa mshindo wa hasira zake
huangamia.
10 [h]Simba anaweza kunguruma na
kukoroma,
lakini bado meno ya simba
mkubwa huvunjika.
11 [i]Simba anaweza kuangamia kwa
kukosa mawindo,
nao wana wa simba jike
hutawanyika.

12 [j]"Neno lililetwa kwangu kwa siri,
masikio yangu yakasikia
mnong'ono wake.
13 [k]Katikati ya ndoto za kutia wasiwasi
wakati wa usiku,
hapo usingizi mzito uwapatapo
wanadamu,
14 [l]hofu na kutetemeka kulinishika
na kufanya mifupa yangu yote
itetemeke.
15 [m]Kuna roho aliyepita mbele ya uso
wangu,
nazo nywele za mwili wangu
zikasimama.
16 [n]Yule roho akasimama,
lakini sikuweza kutambua
kilikuwa kitu gani.
Umbo fulani lilisimama mbele ya
macho yangu,
kukawa na ukimya kisha nikasikia
sauti:
17 [o]'Je, binadamu aweza kuwa
mwadilifu kuliko Mungu?
Je, mtu aweza kuwa safi kuliko
Muumba wake?

[a]**4:3** Sef 3:16; Hos 6:3; Ebr 12:12; Kum 32:2; Ay 29:23; 26:2; Za 71:9; Isa 13:7; 35:3
[b]**4:4** Yer 31:8; Ay 16:5; 29:16, 25; Isa 1:17; 35:3; Ebr 12:12
[c]**4:5** Rut 1:13; Za 38:2; Ay 6:14; Mit 24:10; Lk 4:23
[d]**4:6** Mwa 6:9; Za 71:5; Mit 3:26; Ay 1:1; 1Fal 18:19
[e]**4:7** Za 41:12; 91:9-10; 37:25; 2Pet 2:9; Mit 12:21; Ay 5:11; 36:7; Mt 19:23
[f]**4:8** Amu 14:18; Gal 6:7-8; Hos 8:7; Za 7:14; Yos 1:9; Ay 5:3; 15:17; 5:6; 15:35; Mt 11:18
[g]**4:9** Kut 15:10; 2The 2:8; Law 26:38; Isa 25:7; Ay 41:21; 40:13
[h]**4:10** Ay 38:15; 29:17; Za 22:13; 17:12; 22:21; Mt 28:15
[i]**4:11** Kum 28:41; Mit 30:14; Ay 5:4; Za 34:10; 58:6; Ay 27:14; 29:17
[j]**4:12** Ay 26:14; 33:14; 32:13; 12:23; Yer 9:23; Za 78:59
[k]**4:13** Ay 33:15
[l]**4:14** Dan 10:8; Hab 3:16; Ay 21:6; Za 48:6; 55:5; 119:120, 161; Yer 5:22; 2Kor 7:15
[m]**4:15** Za 104:4; Mt 14:26; Ebr 1:14; Dan 5:6; 7:15, 28; 10:8
[n]**4:16** 1Fal 19:12
[o]**4:17** Za 143:2; Mdo 17:24; Mal 2:10; Mit 20:9; Ay 9:2; 8:3; 10:3; 14:4; 15:14; 13:18; Mhu 7:20; Isa 51:13

[18] [a]Kama Mungu hawaamini watumishi
wake,
kama yeye huwalaumu malaika
zake kwa kukosea,
[19] [b]ni mara ngapi zaidi wale waishio
katika nyumba
za udongo wa mfinyanzi,
ambazo misingi yake ipo
mavumbini,
ambao wamepondwa kama nondo!
[20] [c]Kati ya mawio na machweo
huvunjwa vipande vipande;
bila yeyote kutambua,
huangamia milele.
[21] [d]Je, kamba za hema yao
hazikung'olewa,
hivyo hufa bila hekima?'

*Elifazi Anaendelea*

5 [e]"Ita kama unataka, lakini ni nani
atakayekujibu?
Ni yupi kati ya hao watakatifu
utakayemgeukia?
[2] [f]Kuweka uchungu moyoni humuua
mpumbavu,
nao wivu humchinja mjinga.
[3] [g]Mimi mwenyewe nimemwona
mpumbavu akistawi,
lakini ghafula nyumba yake ikawa
imelaaniwa.
[4] [h]Watoto wake wako mbali na
usalama,
hushindwa mahakamani bila
mtetezi.
[5] [i]Wenye njaa huyala mavuno yake,
wakiyatoa hata katikati ya miiba,
nao wenye kiu huitamani sana
mali yake.
[6] [j]Kwa maana taabu haioti kutoka
kwenye udongo,
wala udhia hauchipui kutoka
ardhini.
[7] [k]Lakini mwanadamu huzaliwa ili
kutaabika,
kwa hakika kama cheche za moto
zirukavyo kuelekea juu.

[8] [l]"Lakini ingekuwa ni mimi,
ningemlalamikia Mungu,
ningeliweka shauri langu mbele
zake.
[9] [m]Yeye hutenda maajabu yasiyoweza
kutambuliwa,
miujiza isiyoweza kuhesabika.
[10] [n]Yeye huipa nchi mvua,
huyapeleka maji kunyesha
mashamba.
[11] [o]Huwainua juu wanyonge,
nao wale waombolezao huinuliwa
wakawa salama.
[12] [p]Huipinga mipango ya wenye hila,
ili mikono yao isifikie ufanisi.
[13] [q]Yeye huwanasa wenye hekima
katika hila yao,
nayo mipango ya wadanganyifu
huifagilia mbali.

[a]**4:18** Ay 25:5; 21:22; 5:4; 1Pet 2:4; Ebr 1:14
[b]**4:19** Isa 64:8; 2Kor 4:7; 2Pet 2:4; Mwa 2:7
[c]**4:20** Za 89:47; 90:5-6; Yak 4:14; Ay 14:2, 20; 15:33; 20:7
[d]**4:21** Ay 8:22; Isa 38:12; Mit 5:23; Yn 8:24; Yer 9:3
[e]**5:1** Ay 15:15; Za 89:5-7; Hab 1:2
[f]**5:2** Mit 12:16; Gal 5:26; Ay 21:15; 36:13
[g]**5:3** Isa 40:24; Eze 17:6; Za 109:9-10; 37:35; 37:22; Mit 3:33; Ay 4:8; 24:18; Yer 12:2; Mit 6:15
[h]**5:4** Ay 20:10; 4:11, 19; Amo 5:12; Za 109:12; Isa 9:17; 1Yn 2:1
[i]**5:5** Law 26:16; Mik 6:15; Amu 2:15; Ay 20:18; 31:8
[j]**5:6** Ay 4:8
[k]**5:7** Mwa 3:17; Mit 22:8; Ay 10:17; 15:35; Za 51:5; 58:3; 90:10
[l]**5:8** Za 50:15; 27:14; 35:23; Ay 8:5; 11:13; 13:3, 15; 13:4; 40:1; Yer 12:1; 1Kor 4:1
[m]**5:9** Za 78:4; 11:2; Kum 29:9; Ay 9:4, 10; 11:7; 25:2; 26:14; Isa 40:28; Rum 11:23
[n]**5:10** Za 135:7; Yer 14:22; Mt 5:45; Law 26:4; Ay 36:28; 37:6, 13
[o]**5:11** 1Sam 2:7-8; Ay 4:7; Za 75:7; 113:7-8; Isa 61:2; Rum 12:5; Yak 4:10; Mt 23:12; 5:4
[p]**5:12** Isa 8:10; Yer 19:7; Neh 4:15; Isa 19:3; Za 33:10; 78:59; Ay 12:23
[q]**5:13** Za 36:3; Lk 20:23; Ay 37:24; Isa 29:14; 44:25; Yer 8:8; 18:18; 51:57; 1Kor 3:19; 2Kor 11:3

14 [a]Giza huwapata wakati wa mchana;
wakati wa adhuhuri hupapasa
kama vile usiku.
15 [b]Humwokoa mhitaji kutokana na
upanga ulioko kinywani
mwao;
huwaokoa kutokana na makucha
ya wenye nguvu.
16 [c]Kwa hiyo maskini analo tarajio,
nao udhalimu hufumba kinywa
chake.

17 [d]"Heri mtu yule ambaye Mungu
humrudi;
kwa hiyo usidharau adhabu yake
Mwenyezi.[e]
18 [f]Kwa kuwa hutia jeraha, lakini pia
huyafunga;
huumiza, lakini mikono yake pia
huponya.
19 [g]Kutoka majanga sita atakuokoa;
naam, hata katika saba hakuna
dhara litakalokupata wewe.
20 [h]Wakati wa njaa atakukomboa wewe
na kifo,
naye katika vita atakukomboa na
pigo la upanga.
21 [i]Utalindwa kutokana na kichapo cha
ulimi,
wala hutakuwa na sababu
ya kuogopa maangamizi
yatakapokujia.
22 [j]Utayacheka maangamizo na njaa,
wala hutakuwa na sababu ya
kuwaogopa
wanyama wakali wa mwituni.
23 [k]Kwa kuwa utakuwa na agano na
mawe ya mashamba,
nao wanyama wa mwitu
watakuwa na amani nawe.
24 [l]Utajua ya kwamba hema lako li
salama;
utahesabu mali zako wala
hutakuta chochote
kilichopungua.
25 [m]Utajua ya kuwa watoto wako
watakuwa wengi,
nao wazao wako wengi kama
majani ya nchi.
26 [n]Utaingia kaburini ukiwa na umri wa
uzee mtimilifu,
kama masuke ya ngano
yakusanywapo kwa wakati
wake.

27 [o]"Tumelichunguza hili, nalo ni
kweli.
Hivyo lisikie na ulitendee kazi."

## HOTUBA YA PILI YA AYUBU

### *Ayubu Anajibu: Malalamiko Yangu Ni Ya Haki*

6 Kisha Ayubu akajibu:

2 [p]"Laiti uchungu wangu
ungeweza kupimwa,
nayo taabu yangu yote ingewekwa
kwenye mizani!
3 [q]Kwa kuwa hakika ingekuwa nzito

---

[a]**5:14** Isa 8:22; Yn 12:35; Amo 8:9; Ay 15:22, 30; 18:6; Kum 28:29
[b]**5:15** Kut 22:23; Ay 4:10; 8:6; 22:27; 33:26; 36:15; 35:10
[c]**5:16** Za 63:11; Rum 3:19; Ay 20:19; 31:16; Mit 17:5; 22:22; Isa 11:4; 41:17; 61:1
[d]**5:17** Sef 3:7; Yak 1:12; Mit 3:11; Yer 31:18; Ebr 12:5-11; Za 94:12; Yak 1:12; Kum 8:5; Ay 33:19; 36:10; Ebr 12:5-11
[e]17 Mwenyezi hapa ni jina la Kiebrania Shaddai (hapa na kila mahali katika kitabu hiki cha Ayubu).
[f]**5:18** Isa 30:26; Kum 32:39; 1Sam 2:6; Isa 57:15; 61:1; Hos 6:1
[g]**5:19** Mit 3:25-26; Kut 12:46; Za 34:19; 91:10; Mit 1:33; 2The 3:3; 2Pet 2:9
[h]**5:20** Ay 5:22; Za 33:19; 22:20; 91:7; 140:7; 144:10; Yer 39:18
[i]**5:21** Za 31:15; 12:2-4; 31:20; 23:4; 27:1; 91:5; Ay 5:15
[j]**5:22** Hos 2:18; Mk 1:14; Ay 8:21; 39:7, 18, 22; 41:29; 5:20; Law 25:18; Za 91:13
[k]**5:23** 2Fal 3:19-25; Mt 13:8; Isa 65:25; Eze 34:25; Za 91:12; Isa 28:15; Hos 2:18; Za 91:12
[l]**5:24** Ay 12:6; 21:9; 8:6; 22:23
[m]**5:25** Kum 28:4; Za 72:16; Isa 48:19; 44:3-4
[n]**5:26** Kum 11:21; Mhu 8:13; Mwa 15:15; Mit 3:21-26
[o]**5:27** Ay 32:10; 8:5; 11:13; 22:27
[p]**6:2** Ay 31:6; Mit 11:1; Dan 5:27
[q]**6:3** Mit 27:3; Ay 21:4; 16:6; 2Fal 4:29; Ay 6:11, 26; 7:11; 16:6

kuliko mchanga wa bahari
zote,
kwa hiyo si ajabu maneno yangu
yamekuwa ya haraka.
4 [a]Mishale ya Mwenyezi iko ndani
yangu,
roho yangu inakunywa sumu yake;
vitisho vya Mungu vimejipanga
dhidi yangu.
5 [b]Je, punda-mwitu hulia akiwa na
majani,
au ng'ombe dume hulia akiwa na
chakula?
6 [c]Je, chakula kisicho na ladha huliwa
bila chumvi,
au upo utamu katika ute mweupe
wa yai?
7 [d]Ninakataa kuvigusa;
vyakula vya aina hii hunichukiza.

8 "Laiti ningepata haja yangu,
kwamba Mungu angenijalia hilo
nililotarajia,
9 [e]kwamba Mungu angekuwa radhi
kuniponda,
kuuachia mkono wake na
kunikatilia mbali!
10 [f]Ndipo bado ningekuwa na hii faraja,
furaha yangu katika maumivu
makali:
kwamba sikuwa nimeyakana
maneno yake yeye Aliye
Mtakatifu.

11 [g]"Ninazo nguvu gani, hata niendelee
kutumaini?
Matazamio yangu ya mbele ni
nini, hata niendelee kuwa
mvumilivu?
12 [h]Je, mimi nina nguvu za jiwe?
Je, mwili wangu ni shaba?
13 [i]Je, ninao uwezo wowote wa
kujisaidia mimi mwenyewe,
wakati ambapo mafanikio
yamefukuziwa mbali nami?

14 [j]"Mtu anayekata tamaa angetazamia
moyo wa kujitoa wa rafiki
zake,
hata kama akiacha uchaji wa
Mwenyezi.
15 [k]Lakini ndugu zangu sio wa
kutegemewa,
ni kama vijito vya msimu,
ni kama vijito ambavyo hufurika
16 [l]wakati vimefunikwa barafu
iyeyukayo,
ambavyo hujazwa na theluji
inayoyeyuka,
17 [m]lakini hukauka majira ya ukame,
na wakati wa hari hutoweka
katika mikondo yake.
18 Misafara hugeuka kutoka njia zake;
hukwea kwenda kwenye nchi ya
ukiwa na kuangamia.
19 [n]Misafara ya Tema inatafuta maji,
wafanyabiashara wa Sheba
wanaosafiri
hutazama kwa matarajio.
20 [o]Wamedhikika, kwa sababu
walikuwa na matumaini;
wanafika huko, lakini
wanahuzunika kwa kukosa
walichotarajia.
21 [p]Sasa nanyi mmethibitika kwamba
hamna msaada wowote;
mnaona jambo la kutisha, nanyi
mnaogopa.

---

[a]**6:4** Kum 32:23; Za 38:2; 88:15-18; Mao 3:12; Ay 16:12-14; Za 7:13; 18:14; 21:12; Mwa 17:1; Ay 7:20; 6:12, 13; Kum 32:32
[b]**6:5** Mwa 16:12; Ay 30:7; 30:24
[c]**6:6** Ay 33:20; Za 107:18
[d]**6:7** Za 31:22
[e]**6:9** 1Fal 19:4; Za 31:22
[f]**6:10** Mk 8:38; Za 119:102; Law 19:2; 2Fal 19:22; Ay 2:11; 15:11; Za 94:19; 38:17; Yer 4:19; 45:3; Ay 22:22; 23:12
[g]**6:11** Ay 6:3
[h]**6:12** Ay 26:2
[i]**6:13** Ay 26:2
[j]**6:14** Ay 4:5; 15:4; 1Sam 20:42; Za 38:11; 69:20; 1Yn 3:17; Mwa 17:1
[k]**6:15** Ay 13:4; 16:2; 21:34; Za 22:1; 38:11; Yer 15:18
[l]**6:16** Za 147:18
[m]**6:17** Ay 24:19
[n]**6:19** Mwa 25:15; Isa 21:14; Mwa 10:7, 28
[o]**6:20** Yer 14:3; Yoe 1:11
[p]**6:21** Za 38:11

22 [a]Je, nimewahi kusema, 'Toeni kitu
kwa ajili yangu,
au mnilipie fidia kutoka mali
zenu,
23 [b]au niokoeni mikononi mwa adui,
au nikomboeni kutoka makucha
ya wasio na huruma'?

24 [c]"Nifundisheni, nami nitanyamaza
kimya;
nionyesheni nilikokosea.
25 [d]Tazama yalivyo ya kuumiza maneno
ya kweli!
Lakini mabishano yenu
yanathibitisha nini?
26 [e]Je, mna maana ya kuyasahihisha
ninayosema,
na kuyafanya maneno ya mtu
anayekata tamaa kama
upepo?
27 [f]Mngeweza hata kupiga kura kwa
ajili ya yatima,
na kubadilishana rafiki yenu na
mali.

28 [g]"Lakini sasa kuweni na huruma
mkaniangalie mimi.
Je, ningeweza kusema uongo
mbele zenu?
29 [h]Tulizeni hasira, msiwe wadhalimu;
angalieni tena, kwa maana
nimehatarisha uadilifu
wangu.[i]
30 [j]Je, pana uovu wowote midomoni
mwangu?
Je, kinywa changu hakiwezi
kupambanua hila?

*Ayubu: Mateso Yangu Hayana Mwisho*

7 [k]"Je, mwanadamu hana kazi ngumu
duniani?
Siku zake si kama zile za mtu
aliyeajiriwa?
2 [l]Kama mtumwa anavyovionea
shauku vivuli vya jioni,
au mtu aliyeajiriwa
anavyoungojea mshahara
wake,
3 [m]ndivyo nilivyogawiwa miezi ya
ubatili,
nami nimeandikiwa huzuni usiku
hata usiku.
4 [n]Wakati nilalapo ninawaza,
'Itachukua muda gani kabla
sijaamka?'
Usiku huwa mrefu, nami
najigeuzageuza hadi
mapambazuko.
5 [o]Mwili wangu umevikwa mabuu na
uchafu,
ngozi yangu imetumbuka na
kutunga usaha.

*Ayubu Anamlilia Mungu*

6 [p]"Siku zangu zinapita upesi kuliko
mtande wa kufuma,
nazo zinafikia mwisho wake bila
matumaini.
7 [q]Kumbuka, Ee Mungu, maisha yangu
ni kama pumzi;
macho yangu kamwe hayataona
tena raha.

---

[a]**6:22** Mdo 20:33; Hes 35:31; Ay 33:24; Za 49:7; Yer 15:10
[b]**6:23** 2Fal 19:19
[c]**6:24** Mit 17:27; Mhu 5:2; Ay 2:10; 33:33; Za 39:1; 141:3; 39:1; Mit 10:19
[d]**6:25** Mhu 12:11; Isa 22:23
[e]**6:26** Mwa 41:6; Yer 5:13; Ay 6:3; 8:2; 15:3; 16:3
[f]**6:27** Nah 3:10; 2Pet 2:3; Eze 24:6; Yoe 3:3; Oba 1:11; Kut 22:22, 24; Isa 10:2; Ay 31:17
[g]**6:28** Ay 9:15; 24:25; 27:4; 34:10; 33:1, 3; 34:6; 36:3, 4
[h]**6:29** Za 66:10; Zek 13:9; Ay 19:6; 27:2; 40:8; Isa 40:27; Ay 2:3; 9:21; 10:7
[i]29 Au: haki yangu bado inasimama.
[j]**6:30** Ay 27:4; 33:8-12; Yak 3:13; Ay 12:11
[k]**7:1** Ay 14:6, 13-14; Isa 40:2; Law 25:50; Za 39:4; Mhu 3:1, 2; Ay 5:7
[l]**7:2** Law 19:13; Ay 14:1; Mhu 2:23; Ay 14:6
[m]**7:3** Mhu 4:1; Mao 1:2, 16; Za 39:5; Mhu 1:14; Isa 16:9; Yer 9:1
[n]**7:4** Kum 28:67; Ay 7:13-14
[o]**7:5** Ay 17:14; Za 38:5-7; Isa 1:6
[p]**7:6** Za 39:5; 52:9; Isa 38:15; Ay 9:25; 13:15
[q]**7:7** Mhu 7:15; Yak 4:14; Ay 9:25; Za 78:39

8 [a]Lile jicho linaloniona sasa
halitaniona tena;
utanitafuta, wala sitakuwepo.
9 [b]Kama vile wingu liondokavyo na
kutoweka,
vivyo hivyo yeye ashukaye
kaburini[c] harudi tena.
10 [d]Kamwe harudi tena nyumbani
mwake;
wala mahali pake hapatamjua
tena.

11 [e]"Kwa hiyo sitanyamaza;
nitanena kutokana na maumivu
makuu ya roho yangu,
nitalalama kwa uchungu wa nafsi
yangu.
12 [f]Je, mimi ni bahari, au mnyama
mkubwa mno akaaye
vilindini,
hata uniweke chini ya ulinzi?
13 [g]Ninapofikiri kwamba kitanda
changu kitanifariji,
nacho kiti changu cha fahari
kitapunguza malalamiko
yangu,
14 [h]ndipo wanitisha kwa ndoto
na kunitia hofu kwa maono,
15 [i]hivyo ninachagua kujinyonga na
kufa,
kuliko huu mwili wangu.
16 [j]Ninayachukia maisha yangu;
nisingetamani kuendelea
kuishi.
Niache; siku zangu ni ubatili.
17 [k]"Mwanadamu ni kitu gani hata
umjali kiasi hiki,
kwamba unamtia sana maanani,
18 [l]kwamba unamwangalia kila asubuhi
na kumjaribu kila wakati?
19 [m]Je, hutaacha kamwe kunitazama,
au kuniacha japo kwa kitambo
kidogo tu?
20 [n]Ikiwa nimetenda dhambi,
nimekufanyia nini,
Ewe mlinzi wa wanadamu?
Kwa nini umeniweka niwe shabaha
yako?
Je, nimekuwa mzigo kwako?
21 [o]Kwa nini husamehi makosa yangu
na kuachilia dhambi zangu?
Kwa kuwa hivi karibuni nitalala
mavumbini;
nawe utanitafuta, wala
sitakuwepo."

*Bildadi Anasema: Yampasa Ayubu Atubu*

8 [p]Kisha Bildadi Mshuhi akajibu:

2 [q]"Hata lini wewe
utasema mambo kama haya?
Maneno yako ni kama upepo
mkuu.
3 [r]Je, Mungu hupotosha hukumu?
Je, Mwenyezi hupotosha kile
kilicho haki?
4 [s]Watoto wako walipomtenda
dhambi,
aliwapa adhabu ya dhambi yao.
5 [t]Lakini ukimtafuta Mungu,
nawe ukamsihi Mwenyezi,

---

[a]**7:8** Isa 41:12; Mdo 20:25; Ay 20:9
[b]**7:9** Ay 30:15; 38:17; 2Sam 12:23; Za 39:13
[c]9 Kaburini hapa maana yake ni Kuzimu, kwa Kiebrania ni Sheol.
[d]**7:10** Ay 18:21; 21:18; 27:21; Za 58:9; Yer 18:17; 19:8; Za 37:10; 104:35
[e]**7:11** Za 39:1, 9
[f]**7:12** Mwa 1:21; Eze 32:2-3; Ay 38:8-11; Isa 1:14
[g]**7:13** Ay 7:11
[h]**7:14** Ay 9:34; 3:26; Mwa 41:8
[i]**7:15** 1Fal 19:4; Yn 4:3; Ay 6:9; Ufu 9:6
[j]**7:16** Mwa 27:46; Za 62:9; 1Fal 19:4; Ay 10:1; Mhu 6:11
[k]**7:17** Za 144:3; 8:4; Ebr 2:6; Ay 4:19
[l]**7:18** Ay 23:10; 14:3; Za 139:23; 17:3; 26:2; 66:10; 73:14
[m]**7:19** Ay 7:16; 9:18; 13:26; 14:6; 27:2; Za 139:7
[n]**7:20** Yer 7:19; Ay 6:4; 16:12; 35:6; Za 36:6
[o]**7:21** Yer 31:34; Mwa 3:19; Ay 9:28; Ebr 1:3; Za 119:120; 7:5; 22:15; 90:3; 104:29; Isa 43:25
[p]**8:1** Mwa 25:2; Ay 18:1; 25:1
[q]**8:2** Ay 6:26; 11:2; 2Nya 36:16
[r]**8:3** Mwa 18:25; 2Nya 19:7; Kum 32:4; Ay 34:12; Dan 9:14
[s]**8:4** Ay 1:5, 18
[t]**8:5** Ay 5:8; 11:13; 22:23

6 [a]ikiwa wewe ni safi na mnyofu,
hata sasa atainuka mwenyewe kwa niaba yako,
na kukurudisha katika mahali pako pa haki.
7 [b]Ijapokuwa mwanzo wako ulikuwa mdogo,
lakini mwisho wako utakuwa wa mafanikio.

8 [c]"Ukaulize vizazi vilivyotangulia
na uone baba zao walijifunza nini,
9 [d]kwa kuwa sisi tumezaliwa jana tu
na hatujui lolote,
nazo siku zetu duniani ni kama kivuli tu.
10 [e]Je, hawatakufundisha na kukueleza?
Je, hawataleta maneno kutoka kwenye kufahamu kwao?
11 [f]Je, mafunjo yaweza kumea mahali pasipo na matope?
Matete yaweza kustawi bila maji?
12 [g]Wakati bado yanaendelea kukua kabla ya kukatwa,
hunyauka haraka kuliko majani mengine.
13 [h]Huu ndio mwisho wa watu wote wanaomsahau Mungu;
vivyo hivyo matumaini ya wasiomjali Mungu huangamia.
14 [i]Lile analolitumainia huvunjika upesi;
lile analolitegemea ni utando wa buibui.
15 [j]Huutegemea utando wake, lakini hausimami;
huung'ang'ania, lakini haudumu.
16 [k]Yeye ni kama mti ulionyeshewa vizuri wakati wa jua,
ukieneza machipukizi yake bustanini;
17 huifunganisha mizizi yake kwenye lundo la mawe,
na kutafuta nafasi katikati ya mawe.
18 [l]Unapong'olewa kutoka mahali pake,
ndipo mahali pale huukana na kusema,
'Mimi kamwe sikukuona.'
19 [m]Hakika uhai wake hunyauka,
na kutoka udongoni mimea mingine huota.

20 [n]"Hakika Mungu hamkatai mtu asiye na hatia,
wala kuitia nguvu mikono ya mtenda mabaya.
21 [o]Bado atakijaza kinywa chako na kicheko,
na midomo yako na kelele za shangwe.
22 [p]Adui zako watavikwa aibu,
nazo hema za waovu hazitakuwepo tena."

### HOTUBA YA TATU YA AYUBU

*Hakuna Mpatanishi*

9 Kisha Ayubu akajibu:

2 [q]"Naam, najua hili ni kweli.
Lakini mwanadamu awezaje kuwa mwadilifu mbele za Mungu?

[a]**8:6** Za 7:6; Isa 58:9; Ay 5:24; 5:15; 22:27; Isa 65:24
[b]**8:7** Ay 21:13; 22:21; 36:11; Za 25:13; Yer 29:11; 31:17
[c]**8:8** Kum 4:32; 32:7; Za 71:18; Ay 15:18
[d]**8:9** Mwa 47:9; 2Nya 10:6; Za 39:5-6; 1Nya 29:15; Ay 7:6
[e]**8:10** Mt 1:8; 2:1-2; 4:1
[f]**8:11** Ay 40:21; Kut 2:3; Isa 19:6; 35:7
[g]**8:12** Isa 34:4; Yer 17:6; Za 129:6; Yak 1:10, 11; 1Pet 1:24
[h]**8:13** Za 50:13; 112:10; Mit 10:28; Yer 15:9; Ay 11:20; 18:14; Isa 33:14; Mt 24:51; Lk 12:1
[i]**8:14** Ay 8:15; 27:18; Isa 59:5
[j]**8:15** Ay 27:18; 8:12; Za 49:11; Mt 7:26-27
[k]**8:16** Za 80:11; 37:35; Isa 16:5; Yer 11:16
[l]**8:18** Ay 14:20; 7:10; Za 37:36; 103:16
[m]**8:19** Za 113:7
[n]**8:20** Mwa 18:25; Ay 21:30; 1The 5:23-24; Za 37:24
[o]**8:21** Ay 5:22; Ezr 3:13; Isa 35:6; Za 47:5; 107:22
[p]**8:22** Za 6:10; Eze 7:27; 1Sam 8:3; Mit 14:11; Ay 18:6
[q]**9:2** Za 143:2; Rum 3:20; Ay 4:17

3 [a]Ingawa mtu angetaka kushindana
naye,
asingaliweza kumjibu Mungu hata
mara moja miongoni mwa
elfu moja.
4 [b]Hekima yake ni kubwa sana na ana
uwezo mwingi mno.
Ni nani aliyempinga naye akawa
salama?
5 [c]Aiondoa milima bila yenyewe kujua
na kuipindua kwa hasira yake.
6 [d]Aitikisa dunia kutoka mahali pake
na kuzifanya nguzo zake
zitetemeke.
7 [e]Husema na jua, nalo likaacha
kuangaza;
naye huizima mianga ya nyota.
8 [f]Yeye peke yake huzitandaza mbingu
na kuyakanyaga mawimbi ya
bahari.
9 [g]Yeye ndiye Muumba wa nyota za
Dubu,[h] na Orioni,[i]
Kilimia,[j] na makundi ya nyota za
kusini.
10 [k]Hutenda maajabu yasiyopimika,
miujiza isiyoweza kuhesabiwa.
11 [l]Anapopita karibu nami, siwezi
kumwona;
apitapo mbele yangu, simtambui.
12 [m]Anapochukua kwa ghafula, ni nani
awezaye kumzuia?
Ni nani awezaye kumwambia,
'Unafanya nini?'
13 [n]Mungu hataizuia hasira yake;
hata jeshi kubwa la Rahabu[o] lenye
nguvu
linajikunyata miguuni pake.

14 [p]"Ni vipi basi mimi nitaweza
kubishana naye?
Nawezaje kupata maneno ya
kuhojiana naye?
15 [q]Ingawa sikuwa na hatia, sikuweza
kumjibu;
ningeweza tu kumsihi Mhukumu
wangu anihurumie.
16 [r]Hata kama ningemwita kwenye
shauri, naye akakubali,
siamini kama angenisikiliza.
17 [s]Yeye angeniangamiza kwa dhoruba
na kuongeza majeraha yangu
pasipo na sababu.
18 [t]Asingeniacha nipumue
bali angenifunika kabisa na huzuni
kuu.
19 [u]Kama ni suala la nguvu, yeye ni
mwenye nguvu!
Kama ni suala la haki, ni
nani awezaye kumwita
mahakamani?
20 [v]Hata kama sikuwa na hatia, kinywa
changu kingenihukumu;
kama sikuwa na kosa,
kingenitangaza kuwa mwenye
hatia.

---

[a]**9:3** Ay 9:32; 40:5; Za 44:21
[b]**9:4** Mit 2:6; 8:6; Mhu 2:26; 2Nya 13:12; Isa 40:26; Ay 5:9; 12:13; Za 93:4; Dan 2:20
[c]**9:5** Isa 13:13; Mik 1:4; Mt 17:20; Za 18:7
[d]**9:6** Hag 2:6; 2:21; Ebr 12:26; Isa 2:19-21; 2Sam 22:8
[e]**9:7** Yer 4:23; Eze 32:8; Isa 34:4; Sef 1:15; Yoe 2:2
[f]**9:8** Mwa 1:1, 8; Isa 48:13; Ay 38:16; Za 77:19; Mit 8:28; Hab 3:15
[g]**9:9** Mwa 1:16; Ay 38:31; 32:22; Amo 5:8
[h]9 Nyota za Dubu hapa ina maana ya kundi la nyota za kaskazini, ambazo zinaitwa kwa jina la Dubu Mkuu.
[i]9 Orioni ni kundi la nyota kubwa.
[j]9 Kilimia ni jina lililopewa nyota saba (Taurus).
[k]**9:10** Kum 6:22; Za 72:18; 136:4; Yer 32:20
[l]**9:11** Ay 23:8-9; 35:14
[m]**9:12** Hes 23:20; Isa 43:13; 14:27; Dan 2:21; Rum 9:20; Ay 11:10
[n]**9:13** Hes 14:18; Ay 10:15; Za 78:38; Isa 3:11; 6:5
[o]13 Rahabu hapa ina maana ya Misri kwa fumbo.
[p]**9:14** Ay 9:3
[q]**9:15** Ay 10:15; 13:19; 34:5-6; 40:5; 42:7; Mwa 18:25; 1Sam 24:12; Za 50:6; 96:13
[r]**9:16** Ay 13:22; Rum 9:20-21
[s]**9:17** Isa 38:13; 38:13; Yn 1:4; Za 10:10; 83:15; Ay 16:12; 30:16; 16:14; 2:3
[t]**9:18** Ay 7:19; 10:1
[u]**9:19** Ay 9:4; Neh 9:32; Yer 49:19
[v]**9:20** Ay 9:15

21 [a]"Ingawa mimi sina kosa,
haileti tofauti katika nafsi yangu;
nauchukia uhai wangu.
22 [b]Hayo yote ni sawa; ndiyo sababu nasema,
'Yeye huwaangamiza wasio na makosa pamoja na waovu.'
23 [c]Wakati pigo liletapo kifo cha ghafula,
yeye hudhihaki kule kukata tamaa kwa yule asiye na kosa.
24 [d]Wakati nchi inapoangukia mikononi mwa waovu,
yeye huwafunga macho mahakimu wake.
Kama si yeye, basi ni nani?

25 [e]"Siku zangu zapita mbio kuliko mkimbiaji;
zinapita upesi bila kuona furaha hata kidogo.
26 [f]Zinapita upesi kama mashua ya mafunjo,
mfano wa tai ayashukiaye mawindo kwa ghafula.
27 [g]Kama nikisema, 'Nitayasahau malalamiko yangu,
nitabadili sura ya uso wangu na kutabasamu,'
28 [h]bado ninahofia mateso yangu yote,
kwa kuwa ninajua hutanihesabu kuwa sina hatia.
29 [i]Kwa kuwa nimeonekana mwenye hatia,
kwa nini basi nitaabishwe bure?
30 [j]Hata kama ningejiosha kwa sabuni
na kutakasa mikono yangu kwa magadi,
31 [k]wewe ungenitupa kwenye shimo la utelezi
kiasi kwamba hata nguo zangu zingenichukia sana.

32 [l]"Yeye si mwanadamu kama mimi ili niweze kumjibu,
ili kwamba tuweze kushindana naye mahakamani.
33 [m]Laiti angelikuwepo mtu wa kutupatanisha kati yetu,
aweke mkono wake juu yetu sote wawili,
34 [n]mtu angeliiondoa fimbo ya Mungu juu yangu,
ili utisho wake usiendelee kunitia hofu.
35 [o]Ndipo ningenena naye, bila kumwogopa,
lakini kama ilivyo kwangu sasa, sitaweza.

### *Ayubu: Nayachukia Maisha Yangu*

10 [p]"Nayachukia sana haya maisha yangu;
kwa hiyo nitatoa malalamiko yangu kwa wazi bila kujizuia,
nami nitanena kutokana na uchungu wa moyo wangu.
2 [q]Nitamwambia Mungu: Usinihukumu,
bali niambie una mashtaka gani dhidi yangu.
3 [r]Je, inakupendeza wewe kunionea,
kuikataa kwa dharau kazi ya mikono yako,
huku wewe ukitabasamu juu ya mipango ya waovu?

---

[a]**9:21** Mwa 6:9; Hes 11:15; Ay 7:15-16; 6:29; 10:1
[b]**9:22** Mhu 9:2-3; Eze 21:3; Ay 3:19
[c]**9:23** Hab 1:3; 1Pet 1:7; Ebr 11:36; Za 64:4
[d]**9:24** Za 73:3; 73:12; Mhu 8:11; Mao 3:9; Ay 1:15, 17; 10:3; 40:8; Yer 12:1; Isa 41:20
[e]**9:25** Ay 7:6, 7; 10:20
[f]**9:26** Isa 18:2; Ay 39:29; Za 46:3; Hab 1:8
[g]**9:27** Ay 7:11
[h]**9:28** Kut 20:7; 34:7; Ay 3:25; 7:21
[i]**9:29** Ay 9:3, 15; Za 37:33
[j]**9:30** Hos 13:12; Isa 1:15-18; Mal 3:2; Ay 31:7; 14:4, 17; 17:9; Yer 2:22
[k]**9:31** Za 35:7; 40:2; 51:9; Yer 2:22; Nah 3:6; Mal 2:3; Ay 7:20
[l]**9:32** Rum 9:20; Mhu 6:10; Za 143:2; Hes 23:19
[m]**9:33** 1Sam 2:25; Ay 9:19
[n]**9:34** Ay 6:4; 21:9; Za 39:10; 73:5; 32:4
[o]**9:35** Ay 7:15; 13:21; 7:11
[p]**10:1** Hes 11:15; 1Sam 1:10; Ay 7:11; 9:18, 21; 1Fal 19:4
[q]**10:2** Ay 13:3; 40:1; Isa 3:13; Hos 4:1; 5:1; Mik 6:2; Rum 8:33
[r]**10:3** Ay 9:24; 22:18; 31:23; Mwa 1:26; Za 138:8; Isa 60:21; 64:8; Za 8:6; 95:6; 100:3

4 [a]Je, wewe una macho ya kimwili?
Je, wewe huona kama
mwanadamu aonavyo?
5 [b]Je, siku zako ni kama zile za
mwanadamu,
au miaka yako ni kama ile ya mtu,
6 [c]ili kwamba utafute makosa yangu
na kuichunguza dhambi yangu;
7 [d]ingawa wajua kuwa mimi sina hatia,
na hakuna awezaye kunitoa
mkononi mwako?

8 [e]"Mikono yako ndiyo iliyoniumba na
kunifanya.
Je, sasa utageuka na
kuniangamiza?
9 [f]Kumbuka kuwa ulinifinyanga kama
udongo wa mfinyanzi.
Je, sasa utanifanya kuwa mavumbi
tena?
10 Je, wewe hukunimimina mimi kama
maziwa,
na kunigandisha kama jibini,
11 [g]ukanivika ngozi na nyama,
na kuniunga pamoja kwa mifupa
na mishipa?
12 [h]Umenipa uhai na kunitendea wema,
katika uangalizi wako umeilinda
roho yangu.

13 [i]"Lakini hili ndilo ulilolificha moyoni
mwako,
nami ninajua kuwa hili lilikuwa
katika nia yako:
14 [j]Kama nilifanya dhambi, ungekuwa
umeniona,
wala usingeacha kosa langu lipite
bila kuadhibiwa.
15 [k]Kama nina hatia, ole wangu!
Hata kama ningekuwa sina hatia,
siwezi kukiinua kichwa changu,
kwa kuwa nimejawa na aibu,
na kuzama katika mateso yangu.
16 [l]Kama nikiinua kichwa changu juu,
unaninyatia kama simba,
na kuonyesha tena uwezo wa
kutisha dhidi yangu.
17 [m]Wewe waleta mashahidi wapya
dhidi yangu
na kuzidisha hasira yako juu
yangu;
nazo nguvu zako zinanijia wimbi
moja baada ya jingine.

18 [n]"Kwa nini basi ulinitoa tumboni?
Ninatamani ningekufa kabla jicho
lolote halijaniona.
19 [o]Laiti nisingekuwako kamwe,
au ningekuwa nimechukuliwa
moja kwa moja
kutoka tumboni kwenda kaburini!
20 [p]Je, siku zangu chache si zimekaribia
kuisha?
Niachie ili niweze kupata muda
mfupi wa kufurahi
21 [q]kabla sijaenda mahali ambapo
hakuna kurudi tena,
katika nchi ya giza na uvuli wa
mauti,
22 [r]nchi ya giza kuu sana,
yenye uvuli wa giza na
machafuko,
mahali ambapo hata nuru ni giza."

---

[a]**10:4** Mit 5:21; Yer 16:17; 1Sam 16:7; Ay 11:11; 14:16; Za 11:4; 33:15; Mit 15:3; Yer 11:20-23
[b]**10:5** Za 102:24; 2Pet 3:8; Ay 36:26; Za 39:5; 90:2, 4
[c]**10:6** Ay 14:16
[d]**10:7** Ay 10:15; 6:29; 11:4; 16:17; Kum 32:39
[e]**10:8** Za 119:73; Isa 43:7; Mwa 2:7; 2Sam 14:14; Ay 30:15
[f]**10:9** Isa 29:16; 64:8; Mwa 2:7; Ay 7:21; 4:19
[g]**10:11** Za 139:13, 15
[h]**10:12** Mwa 2:7; 24:12; 45:5; 1Pet 2:25
[i]**10:13** Ay 23:13; Za 115:3
[j]**10:14** Kut 34:7; Ay 7:21; 13:27
[k]**10:15** Ay 9:13; 10:7; Isa 3:11; Za 25:18; 25:16
[l]**10:16** Yer 5:6; Hos 5:14; 1Sam 28:21; Isa 38:16; Za 7:2; 1Sam 17:38; Mao 3:10
[m]**10:17** 1Fal 21:10; Ay 16:8; Rut 1:21
[n]**10:18** Ay 3:8; 3:26; Za 22:9; Mhu 4:2; 7:1
[o]**10:19** Ay 3:3; Yer 15:10
[p]**10:20** Mhu 6:12; Ay 7:16-19; 5:7; Za 39:13; Ay 9:25
[q]**10:21** 2Sam 12:23; Za 88:12; 23:4; Ay 3:13; Mhu 2:9
[r]**10:22** Ay 3:5; 1Sam 2:9

### *Sofari Anasema: Hatia Ya Ayubu Inastahili Adhabu*

11 [a]Ndipo Sofari Mnaamathi akajibu:
2 [b]"Je, maneno haya yote yapite bila kujibiwa?
Je, huyu mnenaji athibitishwe kuwa na haki?
3 [c]Je, maneno yako ya upuzi yawafanye watu wanyamaze kimya?
Je, mtu asikukemee unapofanya dhihaka?
4 [d]Unamwambia Mungu, 'Imani yangu ni kamili
nami ni safi mbele zako.'
5 Aha! Laiti kwamba Mungu angesema,
kwamba angefungua midomo yake dhidi yako,
6 [e]naye akufunulie siri za hekima,
kwa kuwa hekima ya kweli ina pande mbili.
Ujue hili: Mungu amesahau hata baadhi ya dhambi zako.

7 [f]"Je, waweza kujua siri za Mungu?
Je, waweza kuyachunguza mambo yote kumhusu Mwenyezi?
8 [g]Ni juu mno kuliko mbingu: waweza kufanya nini?
Kina chake ni kirefu kuliko kuzimu:
wewe waweza kujua nini?
9 [h]Kipimo chake ni kirefu kuliko dunia,
nacho ni kipana kuliko bahari.
10 [i]"Kama akija na kukufunga gerezani,
na kuitisha mahakama, ni nani awezaye kumpinga?
11 [j]Hakika anawatambua watu wadanganyifu;
naye aonapo uovu, je, haangalii?
12 [k]Mpumbavu aweza kuwa mwenye hekima,
endapo mtoto wa punda-mwitu atazaliwa mwanadamu.

13 [l]"Hata sasa ukiutoa moyo wako kwake
na kumwinulia mikono yako,
14 [m]ukiiondolea mbali ile dhambi iliyo mkononi mwako
wala usiuruhusu uovu ukae hemani mwako,
15 [n]ndipo utainua uso wako bila aibu;
utasimama imara bila hofu.
16 [o]Hakika utaisahau taabu yako,
utaikumbuka tu kama maji yaliyokwisha kupita.
17 [p]Maisha yako yatang'aa kuliko adhuhuri,
nalo giza litakuwa kama alfajiri.
18 [q]Utakuwa salama, kwa kuwa lipo tumaini;
utatazama pande zote na kupumzika kwa salama.
19 [r]Utalala, wala hakuna atakayekuogofya,
naam, wengi watajipendekeza kwako.

---

[a]**11:1** Ay 2:11
[b]**11:2** Ay 8:2; 16:3; Mwa 41:6
[c]**11:3** Efe 4:29; 5:4; Ay 12:4; 16:10; 17:2; 21:3
[d]**11:4** Ay 6:10; 9:21; 10:7; 1Pet 3:15
[e]**11:6** Ay 9:4; 1Kor 2:10; Mao 3:22; Ezr 9:13
[f]**11:7** Mhu 3:11; Rum 11:33; Isa 40:28; Ay 5:9; Mt 11:27; Efe 3:8
[g]**11:8** Za 57:10; Isa 55:9; Efe 3:18; Mwa 15:5; Ay 22:12; 25:2; Za 57:10; 139:8; Isa 55:9; Ay 7:9; 15:13, 25; 33:13; 40:2
[h]**11:9** Efe 3:19-20; Ay 22:12; 35:5; 36:26; 37:5, 23; Isa 40:26
[i]**11:10** Ay 9:12; Ufu 3:7
[j]**11:11** Ay 10:4; 31:37; 34:11, 25; 36:7; Za 10:14
[k]**11:12** Mwa 12:16; 2Nya 6:36
[l]**11:13** 1Sam 7:3; Za 78:8; 88:9; Kut 9:29; Ay 5:8, 27
[m]**11:14** Yos 24:14; Za 101:4; 22:23
[n]**11:15** Ay 22:26; 1Yn 3:21; 1Tim 2:8; 1Sam 2:9; Za 20:8; 37:23; 40:2; Efe 6:14; Mwa 4:7
[o]**11:16** Isa 26:16; 37:3; 65:16; Eze 21:7; Yos 7:5; Za 58:7; 112:10; Ay 22:11
[p]**11:17** Ay 22:28; Za 37:6; Isa 58:8, 10; 62:1; Ay 17:12; Za 18:28
[q]**11:18** Mhu 5:12; Isa 11:10; Zek 3:10; Za 127:2
[r]**11:19** Law 26:6; Isa 45:14

20 [a]Bali macho ya waovu hayataona,
wokovu utawaepuka;
tarajio lao litakuwa ni hangaiko
la mtu anayekata roho.”

HOTUBA YA NNE YA AYUBU

*Ayubu Anajibu: Mimi Ni Mtu Wa Kuchekwa*

12 Ndipo Ayubu akajibu:

2 [b]“Bila shaka ninyi ndio watu,
nayo hekima itakoma
mtakapokufa!
3 [c]Lakini mimi ninao ufahamu kama
ninyi;
mimi si duni kwenu.
Ni nani asiyejua mambo haya
yote?

4 [d]“Nimekuwa mtu wa kuchekwa na
rafiki zangu,
ingawa nilimwita Mungu naye
akanijibu:
mimi ni mtu wa kuchekwa tu,
ingawa ni mwadilifu na nisiye na
hatia!
5 [e]Wanadamu wakiwa katika utulivu
huwa na dharau kwa wale
wenye msiba
kana kwamba ndiyo haki ya wale
ambao miguu yao inateleza.
6 [f]Hema za wanyang’anyi
hazisumbuliwi,
wale wanaomghadhibisha Mungu
wako salama:
wale wamchukuao mungu wao
mikononi mwao.

7 [g]“Lakini ulizeni wanyama, nao
watawafundisha,
au ndege wa angani, nao
watawaambia;
8 au zungumzeni na dunia, nayo
itawafundisha,
au acheni samaki wa baharini
wawape taarifa.
9 [h]Ni nani miongoni mwa hawa wote
asiyejua
kwamba mkono wa BWANA ndio
uliofanya hili?
10 [i]Mkononi mwake kuna uhai wa kila
kiumbe,
na pumzi ya wanadamu wote.
11 [j]Je, sikio haliyajaribu maneno
kama vile ulimi uonjavyo chakula?
12 [k]Je, hekima haipatikani katikati ya
wazee?
Je, maisha marefu hayaleti
ufahamu?

13 [l]“Hekima na nguvu ni vya Mungu;
shauri na ufahamu ni vyake yeye.
14 [m]Kile anachokibomoa hakiwezi
kujengeka tena;
mtu aliyefungiwa naye hawezi
kufunguliwa.
15 [n]Akizuia maji, huwa pana ukame;
akiyaachia maji, huharibu nchi.
16 [o]Kwake kuna nguvu na ushindi;
adanganywaye na adanganyaye,
wote wawili ni wake.
17 [p]Yeye huwaondoa washauri wakiwa
wametekwa nyara,
naye huwapumbaza wanaotoa
maamuzi.

---

[a]**11:20** Kum 28:65; Yer 11:11; Amo 2:14; Ay 8:13; 17:5
[b]**12:2** Ay 15:8; 17:10
[c]**12:3** Ay 13:2; 15:9
[d]**12:4** Mwa 6:9; 38:23; Ay 21:3; 15:16; Za 91:15
[e]**12:5** Za 123:4; 17:5; 37:31; 38:16; 66:9; 73:2; 94:18; Mit 14:2
[f]**12:6** Ay 5:24; 22:18; 9:24
[g]**12:7** Ay 35:11; 18:3; Mt 6:26; Rum 1:20
[h]**12:9** Isa 41:20; 1:3; Ay 9:24
[i]**12:10** Hes 16:22; Mdo 17:28; Dan 5:23
[j]**12:11** Ay 34:3
[k]**12:12** 1Fal 4:2; Ay 15:10; 17:4; 32:7, 9; 34:4, 10
[l]**12:13** Mit 21:30; Isa 45:9; Yer 32:19; 1Kor 1:24; Dan 1:17
[m]**12:14** Ay 16:9; 9:3; Kum 13:16; Eze 26:14; Ufu 3:7; Za 127:1; Isa 24:20; 25:2
[n]**12:15** 1Fal 8:35; Isa 40:12; Kum 28:22; Mwa 7:11, 14
[o]**12:16** 2Nya 18:22; Rum 2:11; Ay 9:4; 13:7, 9; 27:4
[p]**12:17** Ay 12:19; 19:9; Isa 20:4; Ay 3:14; 1Kor 1:20

18 [a]Huondoa pingu zilizofungwa na
wafalme,
na kuwafunga mishipi ya kiunoni.
19 [b]Huwaondoa makuhani wakiwa
wametekwa nyara,
na kuwaangusha waliojiimarisha
muda mrefu.
20 [c]Hunyamazisha midomo ya washauri
wanaoaminika,
na kuondoa busara ya wazee.
21 [d]Huwamwagia dharau
wanaoheshimika,
na kuwavua silaha wenye nguvu.
22 [e]Hufunua mambo ya ndani ya gizani,
na kuyaleta nuruni yale
yaliyositirika sana.
23 [f]Huyafanya mataifa yatukuke na
kuyaangamiza;
hufanya mataifa kuwa makubwa,
naye huyatawanya.
24 Huwaondolea viongozi wa nchi akili
zao;
huwapeleka watangetange nyikani
pasipo na njia.
25 [g]Hupapasa gizani pasipokuwa na
mwanga;
huwafanya wapepesuke kama
walevi.

13 [h]"Macho yangu yameona hili lote,
masikio yangu
yamesikia na kulielewa.
2 [i]Hayo mnayoyajua mimi pia
ninayajua;
mimi si mtu duni kuliko ninyi.
3 [j]Lakini ninayo shauku ya
kuzungumza na Mwenyezi
na kuhojiana shauri langu na
Mungu.
4 [k]Ninyi, hata hivyo, hunipakaza
uongo;
ninyi ni matabibu wasiofaa kitu,
ninyi nyote!
5 [l]Laiti wote mngenyamaza kimya!
Kwa kuwa kwenu hilo lingekuwa
hekima.
6 [m]Sikieni sasa hoja yangu;
sikilizeni kusihi kwangu.
7 [n]Je, mtazungumza kwa uovu kwa
niaba ya Mungu?
Je, mtazungumza kwa
udanganyifu kwa niaba yake?
8 [o]Mtamwonyesha upendeleo?
Mtamtetea Mungu kwenye
mashtaka yake?
9 [p]Je, ingekuwa vyema Mungu
akiwahoji ninyi?
Je, mngeweza kumdanganya
kama ambavyo mngeweza
kuwadanganya wanadamu?
10 [q]Hakika angewakemea
kama mkiwapendelea watu kwa
siri.
11 [r]Je, huo ukuu wake haungewatisha
ninyi?
Je, hofu yake isingewaangukia
ninyi?
12 [s]Maneno yenu ni mithali za majivu;
utetezi wenu ni ngome za udongo
wa mfinyanzi.

13 [t]"Nyamazeni kimya nipate kusema;
kisha na yanipate yatakayonipata.

---

[a]**12:18** Za 107:14; 116:16; Nah 1:13; Ay 12:21; 34:18
[b]**12:19** Dan 2:21, 34; Kum 24:15; Ay 9:24; 14:20; 22:8; 24:12, 22; 12:17; Isa 2:22
[c]**12:20** Yer 32:9; Kum 4:33-34; Ay 12:12, 24; Dan 4:33-34
[d]**12:21** Ay 12:18; 3:15; Isa 34:12
[e]**12:22** 1Kor 4:5; Ay 3:5; Za 139:12; Dan 2:22
[f]**12:23** Isa 13:4; 54:3; Kut 34:24; Mt 10:26
[g]**12:25** Kum 28:29; Ay 5:14; Za 107:27; Isa 24:20
[h]**13:1** Ay 9:24
[i]**13:2** Ay 12:3
[j]**13:3** Ay 5:8; 23:3-4; 5:17; 40:2
[k]**13:4** Isa 9:15; Yer 23:32; Za 119:69; Yer 8:22; Ay 6:15
[l]**13:5** Mit 17:28; Amo 5:13; Ay 13:13; Amu 18:19; Mhu 5:3; Yak 1:19
[m]**13:6** Ay 33:1; 36:4
[n]**13:7** Ay 16:17; 36:4; 17:5; Rum 3:5-8
[o]**13:8** Law 19:15; Mit 24:23
[p]**13:9** Ay 12:16; 9:3; Gal 6:7
[q]**13:10** Law 19:15; 2Nya 19:7
[r]**13:11** Ay 31:23; Kut 3:6
[s]**13:12** Neh 4:2-3
[t]**13:13** Ay 13:5; 7:11; 9:21

14 [a]Kwa nini nijiweke mwenyewe
kwenye hatari
na kuyaweka maisha yangu
mikononi mwangu?
15 [b]Ingawa ataniua, bado nitamtumaini;
hakika nitazitetea njia zangu
mbele zake.
16 [c]Naam, hili litanigeukia kuwa
wokovu wangu,
kwa maana hakuna mtu asiyemcha
Mungu
atakayethubutu kuja mbele yake!
17 [d]Sikilizeni maneno yangu kwa
makini;
nayo masikio yenu yaingize kile
nisemacho.
18 [e]Sasa kwamba nimekwisha
kutayarisha mambo yangu,
ninajua mimi nitahesabiwa kuwa
na haki.
19 [f]Je, kuna yeyote anayeweza kuleta
mashtaka dhidi yangu?
Kama ndivyo, nitanyamaza kimya
na nife.

20 "Ee Mungu, unijalie tu mimi haya
mambo mawili,
nami sitajificha uso wako:
21 [g]Ondoa mkono wako uwe mbali
nami,
nawe uache kuniogofya kwa hofu
zako kuu.
22 [h]Niite kwenye shauri nami nitajibu,
au niache niseme, nawe upate
kujibu.
23 [i]Ni makosa na dhambi ngapi
nilizotenda?
Nionyeshe kosa langu na dhambi
yangu.
24 [j]Kwa nini kuuficha uso wako
na kunihesabu mimi kuwa adui
yako?
25 [k]Je, utaliadhibu jani lipeperushwalo
na upepo?
Je, utayasaka makapi makavu?
26 [l]Kwa kuwa unaandika mambo
machungu dhidi yangu
na kunifanya nizirithi dhambi za
ujana wangu.
27 [m]Umeifunga miguu yangu kwenye
pingu.
Unazichunga kwa makini njia
zangu zote
kwa kutia alama kwenye nyayo za
miguu yangu.

28 [n]"Hivyo mwanadamu huangamia
kama kitu kilichooza,
kama vazi lililoliwa na nondo.

14 [o]"Mwanadamu aliyezaliwa na
mwanamke
siku zake ni chache nazo zimejaa
taabu.
2 [p]Huchanua kama ua kisha hunyauka;
huwa kama kivuli kipitacho upesi,
wala hadumu.
3 [q]Je, unamwekea jicho lako mtu kama
huyo?
Je, utamleta mbele yako katika
hukumu?
4 [r]Ni nani awezaye kutoa kitu safi
kutoka kitu najisi?
Hakuna awezaye!

---

[a]**13:14** Amu 9:17; Za 119:109
[b]**13:15** Za 27:1; Dan 3:28; Ay 5:8; 27:5; Mit 14:32; Rum 8:38-39
[c]**13:16** Hos 14:4; Flp 1:19; Isa 12:1-2
[d]**13:17** Ay 21:2
[e]**13:18** Ay 13:3; 23:4; 37:19; 2:3; 9:21
[f]**13:19** Isa 50:8; Rum 8:33; Ay 3:13; 40:4; 9:15
[g]**13:21** Za 39:10; Ebr 10:31; Kut 9:3; Ay 6:4
[h]**13:22** Ay 9:35; 14:15
[i]**13:23** 1Sam 26:18; Ay 7:21; 9:21; 14:17; 33:9
[j]**13:24** Isa 8:17; Za 88:14-15; Yer 30:14
[k]**13:25** Law 26:36; Isa 43:17; Hos 13:3
[l]**13:26** Ay 21:23; Za 25:7
[m]**13:27** Mwa 40:15; Mdo 16:24
[n]**13:28** Hos 5:12; Yak 5:2
[o]**14:1** Mhu 2:23; Mwa 3:17; Ay 15:14; 10:20; Mt 11:11; Za 51:5
[p]**14:2** Za 103:15; Yak 1:10; 1Pet 1:24; Isa 40:6-8; Mhu 6:12
[q]**14:3** Za 144:3; 8:4; 143:2; Ay 7:18
[r]**14:4** Mwa 5:3; Ay 4:17; Za 51:10; Rum 5:12; Efe 2:1-3; Yn 3:6

5 [a]Siku za mwanadamu zimewekewa
mpaka;
umekwisha kutangaza idadi ya
miezi yake
na kuweka mpaka ambao hawezi
kuuvuka.
6 [b]Hivyo angalia mbali umwache,
hadi awe amekamilisha muda
wake
kama mtu aliyeajiriwa.

7 [c]"Kwa maana lipo tumaini kwa mti;
kama ukikatwa utachipuka tena,
nayo machipukizi yake mapya
hayatakoma.
8 [d]Mizizi yake yaweza kuchakaa
ardhini
na kisiki chake kufa udongoni,
9 [e]lakini kwa kupata dalili ya maji
utachipua
na kutoa machipukizi kama mche.
10 [f]Lakini mwanadamu hufa, na huo
ndio mwisho wake;
hutoa pumzi ya mwisho, naye
hayuko tena!
11 [g]Kama vile maji yatowekavyo katika
bahari,
au mkondo wa mto ukaushwavyo
na kuwa mkavu,
12 [h]ndivyo mwanadamu alalavyo chini
asiamke;
hadi mbingu zitakapokuwa hazipo
tena,
wanadamu hawataamka au
kuamshwa
kutoka kwenye usingizi wao.

13 [i]"Laiti kama ungenificha kaburini,[j]
na kunisitiri hadi hasira yako
ipite!
Laiti ungeniwekea wakati,
na kisha ukanikumbuka!
14 [k]Je, kama mtu akifa, aweza kuishi
tena?
Siku zote za kazi zangu ngumu
nitangojea kufanywa upya
kwangu.
15 [l]Utaniita nami nitakuitika;
utakionea shauku kiumbe
ambacho mikono yako
ilikiumba.
16 [m]Hakika ndipo utakapozihesabu
hatua zangu,
lakini hutazifuatia dhambi zangu.
17 [n]Makosa yangu yatafungiwa kwa
lakiri kwenye mfuko,
nawe utazifunika dhambi zangu.

18 [o]"Lakini kama mlima
umomonyokavyo na
kufikichika
na kama vile mwamba
uondolewavyo mahali pake,
19 [p]kama maji yamalizavyo mawe,
na mafuriko yachukuavyo udongo,
ndivyo unavyoharibu tegemeo la
mwanadamu.
20 [q]Humshinda mara moja kwa daima,
naye hutoweka;
waibadilisha sura yake na
kumwondoa.

---

[a]**14:5** Ay 24:1; 21:21; Za 31:15; 139:16; 39:4; 90:12; Mdo 17:26
[b]**14:6** Ay 7:19; 7:1, 2; Za 39:13; Isa 16:14; 21:16
[c]**14:7** Ay 19:10; 24:20; Za 52:5; Isa 11:1; 53:2; 60:21; 6:13
[d]**14:8** Isa 6:13; 11:1; 53:2
[e]**14:9** Ay 29:9; Zek 10:1; Za 1:3; Yer 17:8; Eze 31:7; Law 26:4; Eze 34:27
[f]**14:10** Ay 14:12; 10:21; 13:19
[g]**14:11** 2Sam 14:14; Isa 19:5
[h]**14:12** Za 102:26; Ufu 21:1; Mdo 3:21; Ay 14:10; Ufu 20:11
[i]**14:13** Za 30:5; Isa 54:7; Ay 6:8; 7:9; Isa 26:20; 54:7; Mwa 8:1
[j]13 Kaburini hapa maana yake ni Kuzimu, kwa Kiebrania ni Sheol.
[k]**14:14** Ay 7:1; 2Fal 6:33; Za 16:10; 1Kor 15:42-58; Flp 3:21
[l]**14:15** Ay 13:22; Yn 5:28; 1The 4:16; Za 50:4
[m]**14:16** Mit 5:21; Yer 16:17; 32:19; Hos 13:12; 1Kor 13:5
[n]**14:17** Kum 32:34; Ay 13:23; 9:30; Yer 32:10
[o]**14:18** Eze 38:20; Ay 18:4
[p]**14:19** Eze 13:13; Mwa 7:23; Ay 7:8
[q]**14:20** Ay 4:20; 7:10; 8:18; 12:19; 27:19; Yak 1:10

21 [a]Kama wanawe wakipewa heshima,
yeye hafahamu;
kama wakidharauliwa, yeye haoni.
22 [b]Yeye hasikii kingine isipokuwa
maumivu ya mwili wake
mwenyewe,
naye huomboleza kwa ajili yake
mwenyewe."

### *Elifazi Anaongea: Ayubu Anadhoofisha Imani*

15 [c]Kisha Elifazi Mtemani akajibu:

2 [d]"Je, mtu mwenye
hekima hujibu kwa mawazo
matupu,
au kujaza tumbo lake kwa upepo
wenye joto wa mashariki?
3 [e]Je, aweza kubishana juu ya maneno
yasiyofaa,
kwa hotuba zisizo na maana?
4 [f]Lakini unadhoofisha hata uchaji wa
Mungu
na kuzuia ibada mbele za Mungu.
5 [g]Dhambi yako inasukuma kinywa
chako,
nawe umechagua ulimi wa hila.
6 [h]Kinywa chako mwenyewe
kinakuhukumu, wala si
changu;
midomo yako mwenyewe
inashuhudia dhidi yako.

7 [i]"Je, wewe ni mtu wa kwanza
kuzaliwa?
Ulizaliwa kabla ya vilima?
8 [j]Je, wewe husikiliza mashauri ya siri
ya Mungu?
Je, wewe unaizuia hekima iwe
yako mwenyewe?
9 [k]Wewe unajua kitu gani tusichokijua
sisi?
Unafahamu kitu gani
tusichokifahamu sisi?
10 [l]Wale wenye mvi na wazee wako
upande wetu,
watu ambao ni wazee hata kuliko
baba yako.
11 [m]Je, faraja za Mungu hazikutoshi,
au maneno yaliyosemwa kwako
kwa upole si kitu?
12 [n]Kwa nini moyo wako
unakudanganya,
na kwa nini macho yako
yanang'aa,
13 [o]ili kwamba upate kutoa hasira yako
dhidi ya Mungu,
na kumwaga maneno kama hayo
kutoka kinywani mwako?

14 [p]"Mwanadamu ni kitu gani, hata
aweze kuwa safi,
au yeye aliyezaliwa na
mwanamke, hata aweze kuwa
mwadilifu?
15 [q]Kama Mungu hawaamini watakatifu
wake,
kama hata mbingu zenyewe si safi
machoni pake,
16 [r]sembuse mwanadamu ambaye ni
mwovu na mpotovu,
ambaye hunywa uovu kama
anywavyo maji!

17 [s]"Nisikilize mimi nami nitakueleza,
acha nikuambie yale niliyoyaona,

---

[a]**14:21** Mhu 9:5; Isa 63:16; 1Sam 4:20
[b]**14:22** Za 38:7; Isa 21:3; Yer 4:19; Ay 21:21
[c]**15:1** Ay 4:1
[d]**15:2** Mwa 41:6; Ay 6:26
[e]**15:3** Neh 4:2-3; Ay 6:26
[f]**15:4** Ay 25:6
[g]**15:5** Ay 11:6; 22:5; 5:13; Mt 16:23
[h]**15:6** Za 10:2; Mt 12:37; Lk 19:22; Ay 7:15; 18:7
[i]**15:7** Ay 38:21; 1Sam 2:8; Mit 8:25; Za 90:2
[j]**15:8** Yer 23:18; 1Kor 2:11
[k]**15:9** Ay 12:3
[l]**15:10** Ay 12:12; 32:6-7; 8:8-10
[m]**15:11** Mwa 37:35; 2Kor 1:3-4; Kum 8:3; Yer 15:16
[n]**15:12** Ay 11:13; 36:13
[o]**15:13** Mit 29:11; Dan 11:30; Za 94:4; Ay 11:8; 22:5; 30:2
[p]**15:14** Ay 14:1; 4:17; 2Nya 6:36; Mhu 7:18, 20
[q]**15:15** Ay 5:1; 4:18
[r]**15:16** Law 5:2; Ay 12:4; 20:12; Mit 19:28; Za 14:1
[s]**15:17** Ay 4:8

18 [a]ambayo watu wenye hekima
wameyanena,
bila kuficha lolote walilopokea
toka kwa baba zao
19 [b](wakati ambao wao peke yao ndio
walipewa nchi,
hakuna mgeni aliyepita miongoni
mwao):
20 [c]Mtu mwovu siku zake zote hupata
mateso,
miaka yote aliwekewa mkorofi.
21 [d]Sauti za kutisha hujaa masikioni
mwake;
katika kufanikiwa kwake,
wanyang'anyi humshambulia.
22 [e]Hukata tamaa kuokoka gizani;
amewekwa kwa ajili ya upanga.
23 [f]Hutangatanga, akitafuta chakula;
anajua kwamba siku ya giza iko
karibu.
24 [g]Taabu na maumivu makuu vinamtia
hofu;
humshinda kama mfalme aliye
tayari kwa vita,
25 [h]kwa sababu amemkunjia Mungu
ngumi yake
na kujigamba dhidi ya Mwenyezi,
26 [i]kwa kiburi akishambulia dhidi ya
Mungu
akiwa na ngao nene, iliyo imara.

27 [j]"Ingawa uso wake umefunikwa na
mafuta kwa unene
na kiuno chake kimevimba kwa
kunenepa,
28 [k]ataishi katika miji ya magofu,
na katika nyumba ambazo haziishi
mwanadamu yeyote,
nyumba zinazokuwa vifusi.
29 [l]Hatatajirika tena, nao utajiri wake
hautadumu,
wala mali zake hazitakuwa nyingi
juu ya nchi.
30 [m]Hatatoka gizani;
mwali wa moto utanyausha
machipukizi yake,
nayo pumzi ya kinywa cha Mungu
itamwondolea mbali.
31 [no]Asijidanganye mwenyewe
kutumainia ubatili,
kwa kuwa hatapata malipo yoyote.
32 [p]Atakuwa amelipwa kikamilifu kabla
ya wakati wake,
nayo matawi yake hayatastawi.
33 [q]Atafanana na mzabibu
uliopukutishwa matunda yake
kabla hayajaiva,
kama mzeituni unaodondosha
maua yake.
34 [r]Kwa kuwa jamii ya wasiomcha
Mungu watakuwa tasa,
nao moto utateketeza hema za
wale wanaopenda rushwa.
35 [s]Hutunga mimba ya madhara na
kuzaa uovu;
matumbo yao huumba
udanganyifu."

### HOTUBA YA TANO YA AYUBU

*Ayubu Anathibitisha Tena Hali Yake Ya Kutokuwa Na Hatia*

16 Kisha Ayubu akajibu:

2 [t]"Nimepata kusikia
mambo mengi kama haya,
nanyi nyote ni wafariji wenye
kutaabisha!

---

[a]**15:18** Kum 32:7; Ay 8:8; Mwa 18:19
[b]**15:19** Mwa 12:1; Ay 22:8
[c]**15:20** Oba 1:15; Sef 1:17
[d]**15:21** 1Sam 3:11; Yer 6:25; Isa 13:3; 1The 5:3
[e]**15:22** Hos 9:13; Amo 5:19
[f]**15:23** Za 59:15; 109:10; Ay 18:12
[g]**15:24** Isa 8:22; 9:1; Ay 15:20; 18:14
[h]**15:25** Za 2:2-3; Mit 21:30
[i]**15:26** Yer 44:16
[j]**15:27** Amu 3:17; Za 17:10
[k]**15:28** Isa 5:9; Ay 3:14
[l]**15:29** Ay 3:15; 7:8; Isa 5:8
[m]**15:30** Ay 4:9, 15; 16:7; 20:26; Kut 15:10
[n]**15:31** Yer 7:4-8; Mt 6:19; Za 62:10
[o]**15:31** Ay 31:5; Mit 1:16; 6:18; Isa 44:20; 59:7; Mik 2:11; Mk 13:5
[p]**15:32** Mhu 7:17; Za 109:8; Mit 10:27; Ay 18:16
[q]**15:33** Hab 3:17
[r]**15:34** Kut 23:8; Ay 8:22; Isa 33:14
[s]**15:35** Hos 10:13; Gal 6:7; Za 7:14
[t]**16:2** Ay 6:15; 13:4; Za 69:20

3 [a]Je, maneno yenu mengi yasiyo na
maana hayana mwisho?
Mna nini hata mwendelee
kushindana kwa maneno?
4 [b]Mimi pia ningeweza kuzungumza
kama ninyi,
kama mngekuwa katika hali
yangu;
ningeweza kutoa hotuba nzuri dhidi
yenu,
na kuwatikisia ninyi kichwa
changu.
5 [c]Lakini kinywa changu kingewatia
moyo;
faraja kutoka midomoni mwangu,
ingewaletea nafuu.

6 [d]"Lakini kama nikisema, maumivu
yangu bado hayatulizwi;
nami kama nikijizuia, wala
hayaondoki.
7 [e]Ee Mungu, hakika umenichakaza;
umewaangamiza kabisa watu wa
nyumbani mwangu wote.
8 [f]Umenikunjakunja, nalo limekuwa
ushahidi;
nako kukonda kwangu
kumeongezeka sana na
kushuhudia dhidi yangu.
9 [g]Mungu amenishambulia na
kunirarua katika hasira yake,
na kunisagia meno yake;
adui yangu hunikazia macho yake
makali.
10 [h]Watu wamenifumbulia vinywa vyao
kunidhihaki;
hunipiga shavuni mwangu kwa
dharau,
na kuungana pamoja dhidi yangu.
11 [i]Mungu amenigeuzia kwa watu
wabaya,
na kunitupa katika makucha ya
waovu.
12 [j]Mambo yote yalikuwa mazuri, lakini
alinivunjavunja;
amenikamata shingo na
kuniponda.
Amenifanya mimi kuwa shabaha
yake;
13 [k]wapiga upinde wake
wananizunguka.
Bila huruma, huchoma figo zangu,
na kuimwaga nyongo yangu juu
ya nchi.
14 [l]Huniponda tena na tena;
hunishambulia kama shujaa wa
vita.

15 [m]"Nimejishonea nguo ya gunia juu
ya mwili wangu
nami nimekizika kipaji cha uso
wangu kwenye vumbi.
16 [n]Uso wangu umekuwa mwekundu
kwa kulia,
macho yangu yamepigwa na giza
kuu.
17 [o]Hata hivyo mikono yangu
haijafanya jeuri,
na maombi yangu ni safi.

18 [p]"Ee nchi, usiifunike damu yangu,
nacho kilio changu
kisinyamazishwe kamwe.
19 [q]Hata sasa shahidi wangu yuko
mbinguni;
wakili wangu yuko juu.

---

[a]**16:3** Ay 6:26; 11:2; 18:2
[b]**16:4** Mt 27:29; Yer 18:16; Mao 2:15
[c]**16:5** Ay 29:25; Mwa 37:35
[d]**16:6** Ay 6:3; 7:21
[e]**16:7** Amu 8:5; Ay 7:3; 1:19
[f]**16:8** Mao 5:17; Ay 10:17; 17:7; 19:20; Za 22:17; 88:9; 6:7
[g]**16:9** Ay 12:14; 13:24; Mao 2:16; Mdo 7:54; Hos 6:1; Ay 30:21; 9:5; 18:4; 19:11
[h]**16:10** Za 22:13; Mao 3:30; Mdo 7:57; 23:2; Za 27:3; Mik 5:1
[i]**16:11** Ay 9:24
[j]**16:12** Ay 9:17; 6:4; Mao 3:12
[k]**16:13** Mit 7:23; Mao 3:13
[l]**16:14** Ay 9:17; 10:3; Yoe 2:7
[m]**16:15** Mwa 37:34; Ay 2:8
[n]**16:16** Ay 16:20; 2:7; 17:7; 30:17, 30; Isa 52:14; Za 6:6
[o]**16:17** Yer 18:11; Yon 3:8
[p]**16:18** Mwa 4:10; Ay 27:9; Isa 26:21; Za 66:18-19; Ebr 11:4
[q]**16:19** Mwa 31:50; Rum 1:9; 1The 2:5; Ay 22:12; 19:27; Za 113:5; Isa 33:5

20 [a]Mwombezi wangu ni rafiki yangu
macho yangu yamwagapo machozi
kwa Mungu;
21 [b]kwa niaba ya mtu anamsihi Mungu
kama mtu anavyosihi kwa ajili ya
rafiki yake.

22 [c]"Ni miaka michache tu itapita
kabla sijaenda safari ambayo
sitarudi.

17 1 [d]Moyo wangu umevunjika,
siku zangu
zimefupishwa,
kaburi linaningojea.
2 [e]Hakika wenye mizaha
wamenizunguka;
macho yangu yamebaki kutazama
uadui wao.

*Ayubu Anaomba Msaada*

3 [f]"Ee Mungu, nipe dhamana
unayodai.
Ni nani mwingine atakayeweka
dhamana kwa ajili yangu?
4 [g]Umezifunga akili zao zisipate
ufahamu,
kwa hiyo hutawaacha wapate
ushindi.
5 [h]Kama mtu akiwashutumu rafiki
zake ili apate ujira,
macho ya watoto wake
yatashindwa kuona.

6 [i]"Mungu amenifanya kitu cha
dhihaka kwa kila mtu,
mtu ambaye watu humtemea mate
usoni.
7 [j]Macho yangu yamefifia kwa ajili ya
majonzi;
umbile langu lote ni kama kivuli.
8 [k]Watu wanyofu wanatishwa na hili;
watu wasio na hatia wanasimama
dhidi ya wasiomcha Mungu.
9 [l]Hata hivyo, waadilifu watazishika
njia zao,
nao wale wenye mikono safi
wataendelea kupata nguvu.

10 [m]"Lakini ninyi njooni, ninyi nyote,
jaribuni tena!
Sitampata mtu mwenye hekima
miongoni mwenu.
11 [n]Siku zangu zimepita, mipango
yangu imevunjika,
vivyo hivyo shauku za moyo
wangu.
12 [o]Watu hawa hufanya usiku kuwa
mchana,
kwenye giza wao husema,
'Mwanga u karibu.'
13 [p]Kama nyumba pekee ninayoitarajia
ni kaburi,[q]
kama nikikitandika kitanda
changu gizani,
14 [r]kama nikiuambia uharibifu, 'Wewe
u baba yangu,'
na kuliambia buu, 'Wewe u mama
yangu' au 'Dada yangu,'
15 liko wapi basi tarajio langu?
Ni nani awezaye kuona tarajio
lolote kwa ajili yangu?
16 [s]Je, litashuka chini hadi kwenye
malango ya mauti?[t]
Je, tutashuka pamoja
mavumbini?"

---

[a]**16:20** Mao 2:19; Rum 8:34; Yn 15:15; Ay 16:16
[b]**16:21** 1Fal 8:45; Za 140:12
[c]**16:22** Ay 10:21; Mhu 12:5
[d]**17:1** Za 88:3-4; Mhu 12:1-7
[e]**17:2** 1Sam 1:6-7; Ay 11:3
[f]**17:3** Za 35:27; 40:17; Mit 6:1; Isa 38:14
[g]**17:4** Ay 12:12
[h]**17:5** Kut 22:15; Ay 11:20
[i]**17:6** 1Fal 9:7; Yer 15:4
[j]**17:7** Ay 16:8; 2:12; 16:16
[k]**17:8** Kut 4:14; Ay 22:19
[l]**17:9** Mit 4:18; 2Sam 22:21; Ay 22:30
[m]**17:10** Ay 12:3
[n]**17:11** Ay 17:15; Isa 38:10; Ay 7:6
[o]**17:12** Isa 50:11; Ay 5:17-26; 11:17
[p]**17:13** 2Sam 14:14; Ay 3:13; Za 139:8; 88:18
[q]13 Kaburi hapa maana yake ni Kuzimu, kwa Kiebrania ni Sheol.
[r]**17:14** Ay 13:28; 30:28, 30; 4:19; 7:5; Za 16:10; 49:9; 17:15; Ay 7:6; Za 31:23; Mao 3:18; Eze 37:11
[s]**17:16** Mwa 2:7; Yon 2:6; Ay 3:17
[t]16 Malango ya mauti hapa ina maana ya Kuzimu.

*Bildadi Anasema: Mungu Huwaadhibu Waovu*

18 [a]Bildadi Mshuhi akajibu:

2 [b]"Je, ni lini utafika
mwisho wa maneno haya?
Uwe mwenye busara, nasi ndipo
tutakapoweza kuongea.
3 [c]Kwa nini sisi tunafikiriwa kama
wanyama,
na kuonekana wajinga machoni
pako?
4 [d]Wewe unayejirarua mwenyewe
vipande vipande
katika hasira yako,
je, dunia iachwe kwa ajili yako
wewe?
Au ni lazima miamba iondolewe
mahali pake?

5 [e]"Taa ya mwovu imezimwa,
nao mwali wa moto wake
umezimika.
6 [f]Mwanga hemani mwake umekuwa
giza;
taa iliyo karibu naye imezimika.
7 [g]Nguvu za hatua zake
zimedhoofishwa;
shauri lake baya litamwangusha.
8 [h]Miguu yake imemsukumia kwenye
wavu,
naye anatangatanga kwenye
matundu ya wavu.
9 [i]Tanzi litamkamata kwenye kisigino;
mtego utamshikilia kwa nguvu.
10 [j]Kitanzi kimefichwa ardhini kwa ajili
yake;
mtego uko kwenye njia yake.
11 [k]Vitisho vimemtia hofu kila upande,
na adui zake humwandama kila
hatua.
12 [l]Janga linamwonea shauku;
maafa yako tayari kwa ajili yake
aangukapo.
13 [m]Nayo yatakula sehemu ya ngozi
yake;
mzaliwa wa kwanza wa mauti
atakula maungo yake.
14 [n]Atang'olewa kutoka usalama wa
hema lake,
na kupelekwa kwa mfalme wa
vitisho.
15 [o]Moto utakaa katika hema lake;
moto wa kiberiti utamwagwa juu
ya makao yake.
16 [p]Mizizi yake chini itakauka
na matawi yake juu yatanyauka.
17 [q]Kumbukumbu lake litatoweka
katika dunia,
wala hatakuwa na jina katika
nchi.
18 [r]Ameondolewa nuruni na
kusukumiwa gizani,
naye amefukuzwa mbali atoke
duniani.
19 [s]Hana mtoto wala mzao miongoni
mwa watu wake,
wala aliyenusurika mahali
alipoishi.
20 [t]Watu wa magharibi watashangaa
yaliyompata;
watu wa mashariki watapatwa na
hofu.

---

[a]**18:1** Ay 8:1
[b]**18:2** Ay 8:2; 16:3
[c]**18:3** Za 73:22; Ay 12:7
[d]**18:4** Ay 13:14; 16:9; 14:18
[e]**18:5** Yer 25:10; Yn 8:12; Mit 13:9
[f]**18:6** Ay 8:22; 5:14; 11:17; 12:25
[g]**18:7** Za 18:36; Mit 4:12; Ay 5:13; 15:6
[h]**18:8** Mik 7:2; Hab 1:15
[i]**18:9** Ay 22:10; 30:12; Isa 24:18; Yer 48:44; Amo 5:14; Mit 7:22
[j]**18:10** Mit 7:22; Isa 51:20; 1Sam 28:9; Za 140:5
[k]**18:11** Ay 15:21; 20:8; Za 31:13; Isa 22:18; Yer 6:25
[l]**18:12** Isa 9:20; 65:13; 8:21; Ay 21:17; 31:3; 15:25
[m]**18:13** Zek 14:12; Hes 12:12
[n]**18:14** Ay 8:22; 15:24; 18:11
[o]**18:15** Mwa 19:24; Za 11:6; Ay 18:18; 20:26
[p]**18:16** Hos 5:12; Amo 2:9; Mwa 27:28
[q]**18:17** Mit 2:22; 10:7; Isa 49:15; Kum 32:26; 9:14; Za 9:5; 69:28
[r]**18:18** Ay 5:14; 18:11; 11:20; 30:8
[s]**18:19** Za 37:28; 21:10; Isa 14:22; Ay 27:14-15
[t]**18:20** Yer 46:21; Eze 7:7

21 [a]Hakika ndivyo yalivyo makao ya
mtu mwovu;
ndivyo palivyo mahali pake mtu
asiyemjua Mungu."

HOTUBA YA SITA YA AYUBU

*Ayubu Anajibu: Najua Mkombozi Wangu Yu Hai*

19 Ndipo Ayubu akajibu:
2 [b]"Je, mtaendelea
kunitesa mpaka lini,
na kuniponda kwa maneno yenu?
3 [c]Mara kumi hizi mmenishutumu;
bila aibu mnanishambulia.
4 [d]Kama ni kweli nimepotoka,
kosa langu ninabaki kuhusika nalo
mwenyewe.
5 [e]Kama kweli mngejitukuza wenyewe
juu yangu,
na kutumia unyonge wangu dhidi
yangu,
6 [f]basi jueni kuwa Mungu amenitendea
yaliyo mabaya,
naye amekokota wavu wake
kunizunguka.

7 [g]"Ingawa ninalia, 'Nimetendewa
mabaya!' sipati jibu;
ingawa ninaomba msaada, hakuna
haki.
8 [h]Yeye ameizuia njia yangu hivyo
siwezi kupita;
ameyafunika mapito yangu na
giza.
9 [i]Amenivua heshima yangu,
na kuniondolea taji kichwani
pangu.
10 [j]Amenibomoa kila upande hadi
nimeisha;
ameling'oa tegemeo langu kama
mti.
11 [k]Hasira yake imewaka juu yangu;
amenihesabu kuwa miongoni mwa
adui zake.
12 [l]Majeshi yake yananisogelea kwa
nguvu;
yamenizingira,
yamepiga kambi kulizunguka
hema langu.

13 [m]"Amewatenga ndugu zangu mbali
nami;
wale tunaojuana nao
wamefarakana nami kabisa.
14 [n]Watu wa jamaa yangu wamekwenda
mbali;
rafiki zangu wamenisahau.
15 [o]Wageni wangu na watumishi wangu
wa kike wananiona kama
mgeni;
wananitazama kama mgeni.
16 Namwita mtumishi wangu, wala
haitiki,
ingawa namwomba kwa kinywa
changu mwenyewe.
17 [p]Pumzi ya kinywa changu ni kinyaa
kwa mke wangu;
nimekuwa chukizo mno kwa
ndugu zangu mwenyewe.
18 [q]Hata watoto wadogo hunidhihaki;
ninapojitokeza, hunifanyia mzaha.
19 [r]Rafiki zangu wa moyoni wote
wananichukia kabisa;
wale niwapendao wamekuwa
kinyume nami.

---

[a]**18:21** Ay 21:28; Yer 9:3; 1The 4:5
[b]**19:2** 1Sam 1:6; Za 6:2, 3; Ay 6:9; 13:25
[c]**19:3** Mwa 31:7; Ay 20:3
[d]**19:4** Ay 6:24; Za 19:12; Eze 18:4
[e]**19:5** Za 38:16; 55:12; Mik 7:8
[f]**19:6** Ay 6:29; 18:8; 10:3
[g]**19:7** Ay 9:24; 30:20; Za 22:2; Hab 1:2-4
[h]**19:8** Mao 3:7; Hos 2:6; Mhu 6:4; Yer 14:19
[i]**19:9** Ay 12:17; Za 89:39-44; Mao 5:16
[j]**19:10** Ay 12:14; 7:6; 14:7
[k]**19:11** Ay 16:9; 13:14
[l]**19:12** Ay 16:13; 16:10; 3:23
[m]**19:13** Ay 16:10-13; 30:12; Mt 26:56; 2Tim 4:16
[n]**19:14** Ay 19:19; 2Sam 15:12; Ay 12:4; 16:20; Za 88:18; Yer 20:10; 38:22
[o]**19:15** Mwa 14:14; Mhu 2:7
[p]**19:17** Za 38:5
[q]**19:18** 2Fal 2:23; Ay 13:25
[r]**19:19** Za 38:11; 55:12-13; Ay 3:10

20 [a]Mimi nimebaki mifupa na ngozi tu;
nimeponea nikiwa karibu kufa.

21 [b]“Nihurumieni, rafiki zangu, kuweni
na huruma,
kwa kuwa mkono wa Mungu
umenipiga.
22 [c]Kwa nini mnanifuatia kama Mungu
afanyavyo?
Hamtosheki kamwe na mwili
wangu?

23 [d]“Laiti maneno yangu yangewekwa
kwenye kumbukumbu,
laiti kwamba yangeandikwa
kwenye kitabu,
24 [e]kwamba yangechorwa kwenye risasi
kwa kifaa cha chuma,
au kuyachonga juu ya mwamba
milele!
25 [f]Ninajua kwamba Mkombozi[g] wangu
yu hai,
naye kwamba mwishoni
atasimama juu ya nchi.
26 [h]Nami baada ya ngozi yangu
kuharibiwa,
bado nikiwa na mwili huu
nitamwona Mungu;
27 [i]mimi nitamwona kwa macho yangu
mwenyewe:
mimi, wala si mwingine.
Tazama jinsi moyo wangu
unavyomtamani sana!

28 “Kama mkisema, ‘Tazama
tutakavyomwinda,
maadamu mzizi wa tatizo uko
ndani yake,’
29 [j]ninyi wenyewe uogopeni upanga,
kwa kuwa ghadhabu italeta
adhabu kwa upanga,
nanyi ndipo mtakapojua kwamba
kuna hukumu.”

### *Sofari Anasema: Uovu Hupokea Malipo Ya Haki*

20 [k]Ndipo Sofari Mnaamathi akajibu:

2 [l]“Mawazo
yanayonisumbua
yananisukuma kujibu,
kwa sababu nimehangaika sana.
3 [m]Ninasikia makaripio ambayo
yananivunjia heshima,
nao ufahamu wangu unanisukuma
kujibu.

4 [n]“Hakika unajua jinsi ilivyokuwa
tangu zamani,
tangu zamani mwanadamu
alipowekwa duniani,
5 [o]macheko ya mtu mwovu ni ya muda
mfupi,
nayo furaha ya wasiomcha Mungu
hudumu kwa kitambo tu.
6 [p]Ingawa kujikweza kwake hufikia
mbinguni
na kichwa chake hugusa mawingu,
7 [q]ataangamia milele kama mavi yake
mwenyewe.
Wale waliomwona watauliza,
‘Yuko wapi?’
8 [r]Kama ndoto hutoweka, wala
hapatikani tena,
amefukuziwa mbali kama maono
ya usiku.

---

[a]**19:20** Ay 2:5
[b]**19:21** Ay 6:14; Amu 2:15; Ay 4:5; 10:3; Mao 3:1
[c]**19:22** Ay 13:25; 16:11; Mit 30:14; Isa 53:4
[d]**19:23** Kut 17:16; Isa 30:8
[e]**19:24** Yer 17:1; Ay 16:18
[f]**19:25** Law 25:25; Mit 23:11; 1Sam 14:39; Ay 16:19
[g]25 Au: Mtetezi.
[h]**19:26** Hes 12:8; 1Yn 3:2
[i]**19:27** Lk 2:30; Za 42:1; 63:1; 54:2
[j]**19:29** Ay 15:22; Za 58:11; Mhu 12:14
[k]**20:1** Ay 2:11
[l]**20:2** Za 42:5; Mao 1:20
[m]**20:3** Ay 19:3
[n]**20:4** Kum 4:32; Ay 32:7
[o]**20:5** Ay 8:12; Za 73:19; 37:35
[p]**20:6** Ay 33:17; Isa 16:6; Mwa 11:4; Isa 14:13-14; Oba 1:3-4
[q]**20:7** Ay 4:20; 7:8; 14:20
[r]**20:8** Za 90:5; 73:20; Mhu 6:12; 12:7; Ay 18:11-18; Isa 17:14; 29:7

9 [a]Jicho lililomwona halitamwona
tena;
mahali pake hapatamwona tena.
10 [b]Watoto wake watalipa yote baba
yao aliyowadhulumu maskini,
nayo mikono yake itarudisha mali
yote aliyonyang'anya watu.
11 [c]Nguvu za ujana zilizoijaza mifupa
yake,
zitalala naye mavumbini.

12 [d]"Ingawa uovu ni mtamu kinywani
mwake
naye huuficha chini ya ulimi
wake,
13 [e]ingawa hawezi kukubali kuuachia
uende,
lakini huuweka kinywani mwake.
14 [fg]Hata hivyo chakula chake kitakuwa
kichungu tumboni mwake,
nacho kitakuwa sumu kali ya
nyoka ndani yake.
15 [h]Atatema mali alizozimeza;
Mungu atalifanya tumbo lake
kuzitapika.
16 [i]Atanyonya sumu za majoka;
meno ya nyoka mwenye sumu kali
yatamuua.
17 [j]Hatafurahia vijito,
mito inayotiririsha asali na siagi.
18 [k]Vile alivyovitaabikia atavirudisha
bila kuvila;
hatafurahia faida itokanayo na
biashara yake.
19 [l]Kwa kuwa aliwaonea maskini na
kuwaacha pasipo kitu;
amenyang'anya kwa nguvu
nyumba asizozijenga.

20 [m]"Hakika hatakuwa na raha katika
kutamani kwake sana;
hawezi kujiokoa mwenyewe kwa
hazina zake.
21 [n]Hakuna chochote kitakachosalia
kwa ajili yake ili ale;
kufanikiwa kwake hakutadumu.
22 [o]Katikati ya wingi wa ustawi wake,
dhiki itampata;
taabu itamjia kwa nguvu zote.
23 [p]Atakapokuwa amelijaza tumbo lake,
Mungu ataionyesha ghadhabu kali
dhidi yake,
na kumnyeshea mapigo juu yake.
24 [q]Ijapokuwa aikimbia silaha ya
chuma,
mshale wa shaba utamchoma.
25 [r]Atauchomoa katika mgongo wake,
ncha ing'aayo kutoka ini lake.
Vitisho vitakuja juu yake;
26 [s]giza nene linavizia hazina zake.
Moto usiopepewa na mtu
utamteketeza,
na kuangamiza yaliyosalia
nyumbani mwake.
27 [t]Mbingu zitaweka wazi hatia yake,
nayo nchi itainuka kinyume
chake.
28 [u]Mafuriko yataichukua nyumba yake,
maji yaendayo kasi katika siku ya
ghadhabu ya Mungu.

---

[a]**20:9** Ay 7:8
[b]**20:10** Ay 5:4; 20:15, 18, 20; 3:15
[c]**20:11** Ay 13:26; 21:24; 17:16
[d]**20:12** Ay 15:16; Za 10:7; 140:3
[e]**20:13** Hes 11:18-20
[f]**20:14** Za 104:26; Ay 10:18; Mwa 1:21; Ay 41:1, 8, 10, 25
[g]**20:14** Mit 20:17; Yer 2:19; 4:18; Ufu 10:9; Hes 21:6
[h]**20:15** Ay 20:10; Law 18:25
[i]**20:16** Kum 32:24, 34
[j]**20:17** Kum 32:13-14; Ay 29:6; Yer 17:6
[k]**20:18** Ay 20:10; 5:5; Za 109:11
[l]**20:19** Kum 15:11; Amo 8:4
[m]**20:20** Mhu 5:12-14
[n]**20:21** Ay 7:8
[o]**20:22** Amu 2:15; Lk 2:16-20; Ay 20:29; 21:17, 30; 31:2-3
[p]**20:23** Za 78:30-31
[q]**20:24** Yer 46:21; Amo 5:19; Isa 24:18
[r]**20:25** Ay 18:11; 16:13; Za 88:15-16
[s]**20:26** Ay 5:14; 1:16; 15:34; 26:6; 28:22; 31:12; Za 21:9
[t]**20:27** Kum 31:28; Isa 26:21
[u]**20:28** Kum 28:31; Mt 7:26-27; Hes 14:28-32; Efe 5:6

29 [a]Hili ndilo fungu Mungu
alilowagawia waovu,
urithi uliowekwa kwa ajili yao na
Mungu."

HOTUBA YA SABA YA AYUBU

*Ayubu Anajibu: Waovu Mara Nyingi Huenda Bila Kuadhibiwa*

21 Ndipo Ayubu akajibu:
2 [b]"Yasikilizeni maneno
yangu kwa makini;
hii na iwe faraja mnayonipa mimi.
3 [c]Nivumilieni ninapozungumza,
nami nikishazungumza, endeleeni
kunidhihaki.

4 [d]"Je, kwani malalamiko yangu
yanaelekezwa kwa
mwanadamu?
Kwa nini nisikose subira?
5 [e]Niangalieni mkastaajabu;
mkaweke mkono juu ya vinywa
vyenu.
6 [f]Ninapowaza juu ya hili, ninaogopa,
nao mwili wangu unatetemeka.
7 [g]Kwa nini waovu wanaendelea
kuishi,
wakifikia umri wa uzee na
kuendelea kuwa na nguvu?
8 [h]Huwaona watoto wao wakithibitika
wakiwa wamewazunguka,
wazao wao mbele za macho yao.
9 [i]Nyumba zao zi salama wala hakuna
hofu;
fimbo ya Mungu haiko juu yao.
10 [j]Madume yao ya ng'ombe huvyaza
bila kushindwa kamwe;
ng'ombe wao huzaa wala
hawaharibu mimba.
11 [k]Huwatoa watoto wao nje kama
kundi;
wadogo wao huchezacheza.
12 [l]Huimba nyimbo kwa matari na kwa
kinubi,
nao huifurahia sauti ya filimbi.
13 [m]Huitumia miaka yao katika
mafanikio
nao hushuka kaburini kwa amani.
14 [n]Lakini humwambia Mungu, 'Tuache
sisi!'
Hatuna haja ya kufahamu njia
zako.
15 [o]Mwenyezi ni nani hata tumtumikie?
Tutapata faida gani kumwomba?
16 [p]Lakini kufanikiwa kwao hakupo
mikononi mwao wenyewe,
hivyo najitenga mbali na shauri la
waovu.

17 [q]"Lakini ni mara ngapi taa ya waovu
huzimwa?
Ni mara ngapi maafa huwajia,
yale yawapatayo ambayo Mungu
huwapangia katika hasira yake?
18 [r]Ni mara ngapi huwa kama majani
makavu mbele ya upepo,
kama makapi yachukuliwayo na
dhoruba?
19 [s]Imesemekana, 'Mungu huiweka
akiba adhabu ya mtu
kwa ajili ya wanawe.'
Mungu na amlipe mtu mwenyewe,
ili apate kulijua!
20 [t]Macho yake mwenyewe na yaone
maangamizi yake;
yeye na ainywe ghadhabu ya
Mwenyezi.

---

[a]**20:29** Yer 13:25; Kum 29:20, 28; Ufu 21:8; Mt 24:51
[b]**21:2** Ay 13:17; 21:34
[c]**21:3** Ay 6:14; 11:3; 16:10
[d]**21:4** Za 22:1-3; Ay 6:3, 11; 1Sam 1:16
[e]**21:5** Amu 18:19; Ay 40:4
[f]**21:6** Mwa 45:3; Ay 4:14
[g]**21:7** Mhu 7:15; Mal 3:15; Yer 12:1-3
[h]**21:8** Za 17:14; Mal 3:15
[i]**21:9** Ay 5:24; Za 73:5
[j]**21:10** Kut 23:26
[k]**21:11** Za 78:52; 107:41
[l]**21:12** 1Nya 15:16; Mt 15:17
[m]**21:13** Ay 24:19; Za 49:14; Isa 14:15; Ay 3:13
[n]**21:14** Ay 4:17; Kum 32:15; Isa 30:11; 1Sam 11:15
[o]**21:15** Yer 9:6; Mal 3:14
[p]**21:16** Ay 22:18; Za 1:1; 26:5; 36:1
[q]**21:17** Ay 18:5; 18:12; 20:22, 28
[r]**21:18** Ay 13:15; Mwa 19:15; Ay 7:10; Mit 10:25; Mwa 7:23
[s]**21:19** Kut 20:5; Yn 9:2
[t]**21:20** Ay 6:4; Isa 51:17; Yer 25:15; Ufu 14:10

21 [a]Kwani anajali nini kuhusu jamaa
anayoiacha nyuma,
miezi yake aliyopangiwa ifikapo
mwisho?

22 [b]"Je, yuko mtu yeyote awezaye
kumfundisha Mungu maarifa,
iwapo yeye ndiye ahukumuye hata
walio juu ya wote?
23 [c]Mtu mmoja hufa akiwa na nguvu
zake kamili,
akiwa salama na mwenye raha
kamili,
24 [d]mwili wake ukiwa umenawiri,
nayo mifupa yake ikiwa imejaa
mafuta ndani yake.
25 [e]Mtu mwingine hufa katika uchungu
wa nafsi,
akiwa hajafurahia kamwe jambo
lolote zuri.
26 [f]Hao wote hulala mavumbini,
nao mabuu huwafunika wote.

27 "Ninayajua kikamilifu yale
mnayoyafikiri,
mipango ambayo kwayo
mngenitendea mabaya.
28 [g]Mwasema, 'Iko wapi sasa nyumba
ya huyo mtu mkuu,
mahema ambayo watu waovu
walikaa?'
29 Je, hamkuwahi kuwauliza hao
wanaosafiri?
Je, hamkutafakari taarifa zao:
30 [h]kwamba mtu mwovu huepushwa
kutoka siku ya maafa,
kwamba huokolewa kutoka siku
ya ghadhabu?
31 [i]Ni nani hulaumu matendo yake
mbele ya uso wake?
Ni nani ampatilizaye kwa yale
aliyoyatenda?
32 [j]Hupelekwa kaburini,
nao ulinzi ukawekwa kwenye
kaburi lake.
33 [k]Udongo ulio bondeni ni mtamu
kwake;
watu wote watamfuata,
nao umati wa watu usiohesabika
umemtangulia.

34 "Hivyo ninyi mnawezaje kunifariji
kwa upuzi wenu?
Hakuna kilichosalia cha majibu
yenu isipokuwa uongo!"

*Elifazi Anasema: Uovu Wa Ayubu Ni Mkubwa*

22 [l]Ndipo Elifazi Mtemani akajibu:
2 [m]"Je, mwanadamu
aweza kuwa wa faida kwa
Mungu?
Je, hata mtu mwenye hekima
aweza kumfaidi?
3 [n]Je, Mwenyezi angefurahia nini
kama ungekuwa mwadilifu?
Au je, yeye angepata faida gani
kama njia zako zingekuwa
kamilifu?

4 [o]"Je, ni kwa ajili ya utaua wako
ndiyo maana anakukemea
na kuleta mashtaka dhidi yako?
5 [p]Je, uovu wako si mkuu?
Dhambi zako si hazina mwisho?

[a]**21:21** Ay 14:22; 14:5; 14:21; Mhu 9:5-6
[b]**21:22** Za 94:12; 86:8; Rum 11:34
[c]**21:23** Mwa 15:15; Ay 13:26; 3:13
[d]**21:24** Mit 3:8
[e]**21:25** Ay 10:1
[f]**21:26** Mhu 9:2-3; Isa 14:11
[g]**21:28** Ay 1:3; 12:21; 29:25; 31:37; 8:22
[h]**21:30** Ay 31:3; Mit 16:4; Isa 5:30; Rum 5:2
[i]**21:31** Ay 34:11; Za 62:12; Mit 24:11-12; Isa 59:18
[j]**21:32** Isa 14:18
[k]**21:33** Ay 3:17-19; 17:16; 24:24
[l]**22:1** Ay 4:1
[m]**22:2** Lk 17:10; Za 16:2
[n]**22:3** Isa 1:11; Hag 1:8; Za 143:2; Ay 35:7; Za 9:12
[o]**22:4** Isa 3:14; Eze 20:35
[p]**22:5** Ezr 9:13; Ay 11:6; Ezr 9:13; Ay 15:5; 15:13; 20:29; 29:17

6 [a]Umedai dhamana kwa ndugu zako
bila sababu;
umewavua watu nguo zao,
ukawaacha uchi.
7 [b]Hukumpa maji aliyechoka,
nawe ulimnyima chakula mwenye
njaa,
8 [c]ingawa ulikuwa mtu mwenye uwezo
ukimiliki nchi:
mtu uliyeheshimiwa, ukiishi ndani
yake.
9 [d]Umewafukuza wajane mikono
mitupu
na kuzivunja nguvu za yatima.
10 [e]Ndiyo sababu mitego imekuzunguka
pande zote,
hatari ya ghafula inakutia hofu,
11 [f]ndiyo sababu ni giza sana huwezi
kuona,
tena ndiyo sababu mafuriko ya
maji yamekufunika.

12 [g]"Je, Mungu hayuko katika mbingu
za juu?
Juu kuliko nyota zilizo juu sana!
13 [h]Hivyo wewe wasema, 'Mungu
anajua nini?'
Je, yeye huhukumu katika giza
kama hilo?
14 [i]Mawingu mazito ni pazia lake, hivyo
hatuoni sisi
atembeapo juu ya anga la dunia.
15 [j]Je, utaifuata njia ya zamani,
ambayo watu waovu
waliikanyaga?
16 [k]Waliondolewa kabla ya wakati wao,
misingi yao ikachukuliwa na
mafuriko.
17 [l]Walimwambia Mungu, 'Tuache sisi!
Huyo Mwenyezi aweza kutufanyia
nini?'
18 [m]Lakini ndiye alizijaza nyumba zao
na vitu vizuri,
hivyo ninajitenga mbali na
mashauri ya waovu.

19 [n]"Wenye haki wanaona maangamizi
yao na kufurahi,
nao wasio na hatia huwadhihaki,
wakisema,
20 [o]'Hakika adui zetu wameangamizwa,
nao moto umeteketeza mali zao.'

21 [p]"Mjue sana Mungu ili uwe na
amani,
ndipo mema yatakapokujia.
22 [q]Uyapokee mafundisho toka
kinywani mwake,
na maneno yake uyaweke moyoni
mwako.
23 [r]Kama ukimrudia Mwenyezi,
utarudishwa upya:
Kama ukiuondoa uovu uwe mbali
na hema lako,
24 [s]kama dhahabu yako ukiihesabu
kama mavumbi,
dhahabu yako ya Ofiri kama
miamba ya mabondeni,
25 [t]ndipo Mwenyezi atakuwa dhahabu
yako,
naye atakuwa fedha yako iliyo
bora.
26 [u]Hakika ndipo utakapojifurahisha
kwa Mwenyezi,
nawe utamwinulia Mungu uso
wako.

---

[a]**22:6** Kum 24:6, 17; Eze 18:12-16
[b]**22:7** Ay 31:16-17; Eze 18:7; Mt 25:42
[c]**22:8** Ay 15:19; Isa 3:3; 5:13; 9:15; Ay 12:19
[d]**22:9** Isa 10:2; Lk 1:53
[e]**22:10** Ay 18:9; 10:3; 15:21
[f]**22:11** Ay 5:14; Isa 58:10-11; Mao 3:54
[g]**22:12** Ay 11:8; 16:19
[h]**22:13** Eze 9:9; Efe 6:2; Sef 1:12; Za 139:11
[i]**22:14** Ay 26:9; Za 97:2; 105:39; 105:13; 2Fal 21:16; Ay 37:18; Za 18:11; Mit 8:27; Yer 23:23-24
[j]**22:15** Mwa 6:11-13
[k]**22:16** Ay 15:32; Mwa 7:23; Mt 7:26-27
[l]**22:17** Ay 21:15
[m]**22:18** Ay 12:6; 21:16
[n]**22:19** Za 64:10; 97:12; Ay 21:3
[o]**22:20** Ay 15:30
[p]**22:21** Mit 3:10; 1Pet 5:6; Isa 27:5
[q]**22:22** Kum 8:3; Ay 6:10; Eze 3:10; Mit 2:6; Za 37:31
[r]**22:23** Isa 19:22; 44:22; Eze 18:32; Mdo 20:32; Ay 11:14
[s]**22:24** Isa 2:20; 30:22
[t]**22:25** 2Fal 18:7; Mt 6:20-21
[u]**22:26** Za 2:8; Isa 61:10

27 [a]Utamwomba yeye, naye atakusikia,
nawe utazitimiza nadhiri zako.
28 [b]Utakusudia jambo nalo litatendeka,
nao mwanga utaangazia njia zako.
29 [c]Watu watakaposhushwa, nawe
ukasema, 'Wainue!'
ndipo atamwokoa aliyevunjika
moyo.
30 [d]Atamwokoa hata yule ambaye ana
hatia,
ataokolewa kwa sababu ya usafi
wa mikono yako."

## HOTUBA YA NANE YA AYUBU

### *Ayubu Anajibu: Kulalamika Kwangu Ni Uchungu*

23 Ndipo Ayubu akajibu:

2 [e]"Hata leo malalamiko
yangu ni chungu;
mkono wake ni mzito juu yangu
hata nikiugua.
3 [f]Laiti ningefahamu mahali pa
kumwona;
laiti ningeweza kwenda mahali
akaapo!
4 [g]Ningeliweka shauri langu mbele
zake,
na kukijaza kinywa changu na
hoja.
5 Ningejua kwamba angenijibu nini,
na kuelewa lile ambalo
angelisema.
6 [h]Je, angenipinga kwa nguvu nyingi?
La, asingenigandamiza.
7 [i]Hapo mtu mwadilifu angeweka
shauri lake mbele zake,
nami ningeokolewa milele na
mhukumu wangu.
8 "Lakini nikienda mashariki, hayupo;
nikienda magharibi, simpati.
9 [j]Anapokuwa kazini pande za
kaskazini, simwoni;
akigeukia kusini, nako simwoni
hata kidogo.
10 [k]Lakini anaijua njia niiendeayo;
akiisha kunijaribu, nitatoka kama
dhahabu.
11 [l]Nyayo zangu zimefuata hatua zake
kwa karibu;
nimeishika njia yake bila
kukengeuka.
12 [m]Sijaziacha amri zilizotoka
midomoni mwake;
nimeyathamini maneno ya kinywa
chake kuliko chakula changu
cha kila siku.

13 [n]"Lakini yeye husimama peke yake;
ni nani awezaye kumpinga?
Yeye hufanya lolote atakalo.
14 [o]Hutimiliza maagizo yake dhidi
yangu,
na bado anayo mipango mingi
kama hiyo ambayo ameiweka
akiba.
15 [p]Hiyo ndiyo sababu ninaingiwa na
hofu mbele zake;
nifikiriapo haya yote
ninamwogopa.
16 [qr]Mungu ameufanya moyo wangu
kuzimia;
yeye Mwenyezi amenitia hofu.

---

[a]**22:27** Ay 5:27; Isa 58:9
[b]**22:28** Za 103:11; 145:19; Ay 33:28; Mit 4:18; Za 97:11
[c]**22:29** Za 18:27; 1Pet 5:5
[d]**22:30** 2Sam 22:21; Ay 42:7-8
[e]**23:2** Ay 6:3; 7:11; 1Sam 1:10
[f]**23:3** Kum 4:29
[g]**23:4** Ay 13:18; 9:15
[h]**23:6** Ay 9:4, 19; Isa 27:4
[i]**23:7** Mwa 3:8; Ay 9:3
[j]**23:9** Ay 9:11
[k]**23:10** Za 66:10; 139:1-3; 12:6; 1Pet 1:7; Yak 1:12
[l]**23:11** Za 17:5; Ay 31:7; Yer 11:20; Za 44:18; 125:5
[m]**23:12** Ay 6:10; 15:11; Yn 4:32, 34; Mt 4:4
[n]**23:13** Za 115:3; Isa 55:11; Mhu 3:14; Rum 9:19
[o]**23:14** 1The 3:3; 1Pet 4:12
[p]**23:15** Mwa 45:3; Yos 24:14; Mhu 3:14; 12:13; 2Kor 5:11
[q]**23:16** Za 22:14; Yer 51:46; Ay 27:2
[r]**23:16** Kum 20:3; Ay 27:2; Kut 3:6; Ufu 6:16

17 [a]Hata hivyo sijanyamazishwa na
giza,
wala kwa giza nene linalofunika
uso wangu.

*Ayubu Analalamikia Jeuri Duniani*

24 [b]"Kwa nini Mwenyezi asiweke
nyakati kwa ajili ya hukumu?
Kwa nini wale wamjuao
wazitafute siku kama hizo
bila mafanikio?
2 [c]Watu husogeza mawe ya mpaka;
huchunga makundi ya wanyama
waliyonyang'anya kwa nguvu.
3 [d]Huwanyang'anya yatima punda
wao,
na kumchukua rehani fahali wa
mjane.
4 [e]Humsukuma mhitaji kutoka njia,
na kuwafanya maskini wote wa
nchi kulazimika kujificha.
5 [f]Kama punda-mwitu jangwani,
maskini huzunguka katika kazi
zao za kutafuta chakula;
mahali palipo jangwa
huwapa chakula cha watoto wao.
6 [g]Hukusanya chakula mashambani na
kuokota masazo
katika mashamba ya mizabibu ya
waovu.
7 [h]Kwa kukosa nguo, usiku kucha
hukaa uchi;
hawana chochote cha kujifunika
baridi.
8 [i]Hutota kwa mvua za mlimani,
nao huikumbatia miamba kwa ajili
ya kukosa pa kujisitiri.
9 [j]Mtoto yatima hupokonywa matitini;
mtoto wachanga wa maskini
hunyakuliwa kwa ajili ya
deni.
10 [k]Kwa kukosa nguo, hutembea uchi;
hubeba miganda ya ngano, lakini
huwa na njaa.
11 [l]Hukamua zeituni katika mawe ya
kusagia;
hukanyaga mashinikizo, lakini
wanaona kiu.
12 [m]Kilio cha huzuni cha wanaokufa
kinapaa kutoka mjini,
nazo nafsi za waliojeruhiwa
zinalilia msaada.
Lakini Mungu hamlaumu mtu yeyote
kwa kutenda mabaya.

13 [n]"Wako wale wanaoiasi nuru,
wasiofahamu njia zake
wala hawakai katika mapito yake.
14 [o]Wakati mwanga wa mchana
unapotoweka, muuaji huinuka
naye huwaua maskini na mhitaji;
wakati wa usiku hunyemelea
kama mwizi.
15 [p]Jicho la mzinzi hungojea wakati wa
giza,
naye hufikiri, 'Hakuna jicho
litakaloniona,'
naye huuficha uso wake.
16 [q]Katika giza, huvunja majumba,
lakini wakati wa mchana
hujifungia ndani;
hawataki kufanya lolote nuruni.
17 [r]Kwa wote hawa, giza nene ndiyo
asubuhi yao;
hujifanya rafiki na vitisho vya
gizani.

---

[a]**23:17** Ay 3:6; 6:9; 19:8
[b]**24:1** Yer 46:10; 2Pet 3:7; Ay 15:20; Mdo 1:7
[c]**24:2** Kum 19:14; 27:17; Mit 23:10
[d]**24:3** Kum 24:6-10; 12:17; Ay 6:27
[e]**24:4** Mit 28:28; Ay 20:19; Isa 11:4; Za 12:5
[f]**24:5** Mwa 16:12; Za 104:23; Ay 30:3
[g]**24:6** Ay 6:5; Rut 2:22; 1Fal 21:19
[h]**24:7** Kut 22:26-27; Kum 24:12; Ay 22:6
[i]**24:8** Dan 4:25, 33; Mao 4:5
[j]**24:9** Kum 24:17
[k]**24:10** Kum 24:12-13; Law 19:9
[l]**24:11** Isa 5:2; 16:10; Hag 2:16; Mik 6:15
[m]**24:12** Isa 30:19; Ay 9:23; Ufu 6:10; Mhu 8:11
[n]**24:13** Ay 38:15; 1The 5:4-5; Za 18:28; Efe 5:8-14
[o]**24:14** Isa 3:15; Mik 3:3; Ay 20:19; Za 37:32; 10:9
[p]**24:15** Mit 7:8-9; Za 10:11
[q]**24:16** Kut 22:2; Mt 6:19; Yn 3:20
[r]**24:17** Ay 18:11; 15:22; 18:5

18 [a]"Lakini wao ni povu juu ya maji;
sehemu yao juu ya nchi
imelaaniwa,
hivyo hakuna hata mmoja
aendaye kwenye shamba la
mizabibu.
19 [b]Kama vile joto na hari vinyakuavyo
theluji iliyoyeyuka,
ndivyo kuzimu kuwanyakuavyo
waliotenda dhambi.
20 [c]Tumbo lililowazaa huwasahau,
nao huwa karamu ya mabuu;
watu waovu hawakumbukwi tena,
lakini huvunjika kama mti.
21 [d]Huwafanya mawindo wanawake
tasa na wasio na watoto,
nao hawaonyeshi huruma kwa
wajane.
22 [e]Lakini Mungu huwakokota wenye
nguvu kwa uwezo wake;
ingawa wamestawi, hawana
hakika ya maisha.
23 [f]Aweza akawaacha wakapumzika
wakijihisi salama,
lakini macho yake yanaona njia
zao.
24 [g]Kwa kitambo kidogo hutukuka,
hatimaye hutoweka;
hushushwa na kukusanywa kama
wengine wote,
hukatwa kama masuke ya nafaka.

25 [h]"Kama hili sivyo, ni nani awezaye
kunithibitisha kuwa mwongo,
na kuyafanya maneno yangu kuwa
si kitu?"

*Bildadi Anasema: Mwanadamu Awezaje Kuwa Mwadilifu Mbele Za Mungu?*

25 [i]Ndipo Bildadi Mshuhi akajibu:

2 [j]"Mamlaka na
kuheshimiwa ni vyake
Mungu;
yeye huthibitisha amani katika
mbingu juu.
3 [k]Je, majeshi yake yaweza
kuhesabika?
Ni nani asiyeangaziwa na nuru
yake?
4 [l]Mtu awezaje kuwa mwadilifu mbele
za Mungu?
Awezaje mtu aliyezaliwa na
mwanamke kuwa safi?
5 [m]Ikiwa hata mwezi sio mwangavu
nazo nyota si safi machoni pake,
6 [n]sembuse mtu ambaye ni funza:
mwanadamu ambaye ni buu tu!"

## HOTUBA YA TISA YA AYUBU

*Ayubu Anajibu: Utukufu Wa Mungu Hauchunguziki*

26 Kisha Ayubu akajibu:

2 [o]"Tazama jinsi
ulivyomsaidia mtu asiye na
uwezo!
Jinsi ulivyouokoa mkono ulio
dhaifu!
3 [p]Ni shauri gani ulilompa yeye asiye
na hekima?
Nayo ni busara gani kubwa
uliyoonyesha!
4 [q]Ni nani aliyekusaidia kutamka
maneno hayo?
Nayo ni roho ya nani iliyosema
kutoka kinywani mwako?

---

[a]**24:18** Ay 9:26; 22:16; Yud 23; Isa 57:20
[b]**24:19** Ay 6:17; 21:13
[c]**24:20** Ay 18:17; Mit 10:7; Dan 4:14; Za 31:12
[d]**24:21** Ay 22:9
[e]**24:22** Kum 28:66; Mt 6:27
[f]**24:23** Ay 9:24; Amo 6:1; 2Nya 16:9; Ay 10:4
[g]**24:24** 2Fal 19:35; Za 37:35-36; 83:13; Isa 17:5
[h]**24:25** Ay 16:17; 27:4
[i]**25:1** Ay 8:1
[j]**25:2** Zek 9:2; Ufu 1:6
[k]**25:3** Mt 5:45; Yak 1:17; Mwa 1:14-16
[l]**25:4** Ay 4:17; 14:4; Rum 3:19-20
[m]**25:5** Ay 31:26; 4:18
[n]**25:6** Za 22:6; 80:17; Eze 2:1; Ay 7:5
[o]**26:2** Ay 6:12; 4:3; Za 71:9; Mit 25:11
[p]**26:3** Ay 34:35
[q]**26:4** 1Fal 22:24

5 [a]"Wafu wako katika maumivu
makuu,
wale walio chini ya maji na wale
waishio ndani yake.
6 [b]Mauti[c] iko wazi mbele za Mungu;
Uharibifu[d] haukufunikwa.
7 [ef]Hutandaza anga la kaskazini mahali
patupu;
naye huining'iniza dunia mahali
pasipo na kitu.
8 [g]Huyafungia maji kwenye mawingu
yake,
hata hivyo mawingu hayapasuki
kwa uzito wake.
9 [h]Huufunika uso wa mwezi mpevu,
akitandaza mawingu juu yake.
10 [i]Amechora mstari wa upeo juu ya
uso wa maji,
ameweka mpaka wa nuru na giza.
11 [j]Nguzo za mbingu nazo zatetemeka,
zinatishika anapozikemea.
12 [k]Kwa nguvu zake aliisukasuka
bahari;
kwa hekima yake alimkata
Rahabu[l] vipande vipande.
13 [m]Aliisafisha anga kwa pumzi yake;
kwa mkono wake alimchoma joka
aendaye mbio.
14 [n]Haya ni mambo madogo tu katika
matendo yake;
tazama jinsi ulivyo mdogo
mnong'ono tunaousikia
kumhusu!
Ni nani basi awezaye kuelewa
ngurumo za nguvu zake?"

## HOTUBA YA MWISHO YA AYUBU

### *Ayubu Anadumisha Uadilifu Wake*

27 [o]Ndipo Ayubu akaendelea na hoja
yake, akasema:

2 [p]"Hakika kama Mungu aishivyo,
aliyeninyima haki yangu,
Mwenyezi ambaye amenifanya
nionje uchungu wa nafsi,
3 [q]kwa muda wote nitakaokuwa na
uhai ndani yangu,
nayo pumzi ya Mungu ikiwa puani
mwangu,
4 [r]midomo yangu haitanena uovu,
wala ulimi wangu hautatamka
udanganyifu.
5 [s]Sitakubaliana nanyi kabisa kuwa
mko sahihi;
hadi nife, sitakana uadilifu wangu.
6 [t]Nitadumisha haki yangu wala
sitaiacha;
dhamiri yangu haitanisuta muda
wote ninaoishi.

7 "Watesi wangu wawe kama waovu,
nao adui zangu wawe kama wasio
haki!
8 [u]Kwa maana mtu asiyemcha Mungu
analo tegemeo gani anapokatiliwa
mbali,
Mungu anapouondoa uhai wake?
9 [v]Je, Mungu husikiliza kilio chake,
shida zimjiapo?
10 [w]Je, anaweza kumfurahia Mwenyezi?
Je, atamwita Mungu nyakati zote?

---

[a]**26:5** Za 88:10; Isa 14:9
[b]**26:6** Za 139:8; Mit 15:11; Ebr 4:13; Amo 9:2
[c]6 Yaani Kuzimu; Kiebrania ni Sheol.
[d]6 Kwa Kiebrania ni Abadon.
[e]**26:7** Ay 9:8
[f]**26:7** Ay 8:22; 31:35
[g]**26:8** Mit 30:4; Za 147:8
[h]**26:9** 2Sam 22:10; Za 97:2
[i]**26:10** Mit 8:27; Isa 40:22; Ay 28:3
[j]**26:11** 2Sam 22:8
[k]**26:12** Isa 51:15; Kut 14:21; Yer 31:35; Ay 12:13; Kut 14:21; Ay 12:13; 9:13
[l]12 Rahabu hapa ni fumbo la kumaanisha Lewiathani, mnyama mkubwa wa baharini mwenye magamba anayefanana na joka kubwa, mwenye umbo la kutisha, asiyeweza kuvuliwa.
[m]**26:13** Za 33:6; Isa 27:1
[n]**26:14** Ay 9:6; 36:29
[o]**27:1** Ay 29:1
[p]**27:2** Ay 9:18; 34:5; Isa 45:9; 1Sam 1:10
[q]**27:3** Mwa 2:7; Za 144:4
[r]**27:4** Ay 6:28; 12:16; 16:17
[s]**27:5** Ay 2:9; 10:7; 32:2
[t]**27:6** Ay 29:14; Za 119:121; Isa 59:17; 61:10; Rum 2:15
[u]**27:8** Ay 8:13; Hes 16:22; Lk 12:20; Mt 16:26
[v]**27:9** Zek 7:13; Mik 3:4; 1Sam 8:18
[w]**27:10** Ay 22:26

11 [a]"Nitawafundisha juu ya uweza wa
Mungu;
njia za Mwenyezi sitazificha.
12 Ninyi nyote mmeona hili wenyewe.
Ni ya nini basi mazungumzo haya
yasiyo na maana?

13 [b]"Hili ndilo fungu ambalo Mungu
humpa mtu mwovu,
urithi ule mtu mdhalimu anapokea
kutoka kwa Mwenyezi:
14 [c]Hata kama watoto wake watakuwa
wengi kiasi gani,
fungu lao ni kuuawa kwa upanga;
wazao wake hawatakuwa kamwe
na chakula cha kuwatosha.
15 [d]Tauni itawazika wale
watakaonusurika miongoni
mwao,
nao wajane wao
hawatawaombolezea.
16 [e]Ajapokusanya fedha nyingi kama
mavumbi,
na mavazi kama malundo ya
udongo wa mfinyanzi,
17 [f]yale yote mtu mwovu aliyojiwekea
akiba, mwenye haki atayavaa,
naye asiye na hatia ataigawanya
fedha yake.
18 [g]Nyumba aijengayo ni kama utando
wa buibui,
kama kibanda alichotengeneza
mlinzi.
19 [h]Yeye hulala akiwa tajiri, lakini
ndiyo mara ya mwisho;
afunguapo macho yake, yote
yametoweka.
20 [i]Vitisho humjia kama mafuriko;
dhoruba humkumba ghafula usiku.
21 [j]Upepo mkali wa mashariki
humchukua, naye hutoweka;
humzoa kutoka mahali pake.
22 [k]Humvurumisha bila huruma,
huku akikimbia kasi kukwepa
nguvu zake.
23 [l]Upepo humpigia makofi kwa
dharau,
na kumfukuza atoke mahali pake.

### *Mapumziko: Imani Inakopatikana*

28 [m]"Kuna machimbo ya fedha,
na mahali dhahabu
isafishwapo.
2 [n]Chuma hupatikana ardhini,
nayo shaba huyeyushwa kutoka
mawe ya madini.
3 [o]Mwanadamu hukomesha giza;
huyatafuta hadi sehemu iliyo
mbali,
kwa ajili ya kuchimbua mawe yenye
madini
katika giza jeusi sana.
4 [p]Huchimba shimo jembamba mbali
na makao ya watu,
mahali paliposahaulika na nyayo
za wanadamu;
mbali na wanadamu huning'inia
na kupembea kwa kamba.
5 [q]Ardhi, ambako chakula hutoka,
chini hugeuzwa kwa moto;
6 [r]yakuti samawi hutoka katika
miamba yake,
nalo vumbi lake lina vipande vya
dhahabu.

---

[a]**27:11** Ay 36:23; 27:13
[b]**27:13** Ay 15:20; 16:19
[c]**27:14** Mao 2:22; Es 9:10; Hos 9:13; Ay 20:10; 2Fal 10:6-10
[d]**27:15** Za 78:64
[e]**27:16** Zek 9:3
[f]**27:17** Mit 13:22; Mhu 2:26
[g]**27:18** Ay 8:14; Isa 1:8; 24:20; Mao 2:6
[h]**27:19** Ay 3:13; Hes 20:26
[i]**27:20** Ay 15:21; 20:8
[j]**27:21** Ay 38:24; Yer 13:24; Ay 30:22; 7:10; Yer 22:22
[k]**27:22** Yer 13:14; Eze 5:11; Ay 11:20
[l]**27:23** Ay 7:10; 18:18
[m]**28:1** Za 12:6; 66:10; Yer 9:7; Mal 3:3; Dan 11:35
[n]**28:2** Kum 8:9
[o]**28:3** Mhu 7:25; 8:17; Mit 2:4
[p]**28:4** 2Sam 5:8
[q]**28:5** Mwa 1:29; Za 145:15
[r]**28:6** Isa 54:11; Wim 5:14; Ay 22:24

7 [a]Hakuna ndege awindaye aijuaye
njia ile iliyofichika,
wala hakuna jicho la mwewe
lililoiona.
8 [b]Wanyama wa porini wanaotamba
hawajawahi kupakanyaga,
wala simba azungukaye huko.
9 [c]Mikono ya mwanadamu
hushambulia miamba migumu
sana,
na kuiacha wazi mizizi ya milima.
10 [d]Hutoboa shimo refu la kupenya
chini kwa chini kwenye
miamba;
macho yake huona hazina zake
zote.
11 [e]Hutafuta vyanzo vya mito
na kuvileta vitu vilivyofichika
katika nuru.

12 [f]"Lakini hekima inaweza kupatikana
wapi?
Ufahamu unakaa wapi?
13 [g]Mwanadamu hatambui thamani
yake;
haiwezi kupatikana katika nchi ya
walio hai.
14 Kilindi husema, 'Haiko ndani yangu';
bahari nayo husema, 'Haiko
pamoja nami.'
15 [h]Haiwezi kununuliwa kwa dhahabu
safi kuliko zote,
wala thamani yake haiwezi
kupimwa kwa fedha.
16 Haiwezi kununuliwa kwa dhahabu
ya Ofiri,
kwa shohamu ya thamani kubwa
au yakuti samawi ya thamani
kubwa.
17 [i]Dhahabu wala mawe maangavu
haviwezi kulinganishwa nayo,
wala haiwezi hubadilishwa na vito
vya dhahabu.
18 Marijani na yaspi hazistahili
kutajwa;
thamani ya hekima ni zaidi ya
akiki nyekundu.
19 [j]Yakuti manjano ipatikanayo Kushi
haiwezi kulinganishwa nayo,
wala haiwezi kununuliwa kwa
dhahabu safi.

20 "Ni wapi basi hekima itokako?
Ufahamu hukaa wapi?
21 [k]Imefichika machoni pa kila kitu
kilicho hai,
imesitiriwa hata kwa ndege wa
angani.
22 [l]Uharibifu na Mauti husema,
'Ni uvumi wake tu uliotufikia
masikioni mwetu.'
23 [m]Mungu anaifahamu njia ya
kuiendea hekima
na ndiye peke yake anayefahamu
inakokaa,
24 [n]kwa maana yeye huitazama miisho
ya dunia
na huona kila kitu chini ya
mbingu.
25 [o]Alipofanyiza nguvu za upepo
na kuyapima maji,
26 [p]alipofanya maagizo kwa ajili ya
mvua
na njia kwa ajili ya umeme wa
radi,
27 ndipo alipoitazama hekima na
kuikadiria thamani yake,
akaithibitisha na kuihakikisha.

[a]**28:7** Ay 28:21
[b]**28:8** Ay 41:34; Isa 35:9
[c]**28:9** Kum 8:15; Yn 2:6
[d]**28:10** Mit 2:4; Ay 28:4
[e]**28:11** Mwa 7:11; Isa 48:6; Yer 33:3
[f]**28:12** Mit 1:20; Mhu 7:24
[g]**28:13** Mit 3:15; Mt 13:44-46
[h]**28:15** Mit 16:16; Mdo 8:20
[i]**28:17** Za 119:72; Mit 8:10; Ay 28:15
[j]**28:19** Mit 3:14-15; 8:10-19
[k]**28:21** Ay 28:7
[l]**28:22** Ay 26:6
[m]**28:23** Mdo 15:18; Ay 22:22; Mit 8:22-31
[n]**28:24** Isa 11:12; Yos 3:11; Ebr 4:13; Za 66:7
[o]**28:25** Ay 38:8-11; Za 135:7
[p]**28:26** Ay 38:25-27; Isa 35:7; Yer 14:22

28 [a]Naye Mungu akamwambia
mwanadamu,
'Kumcha BWANA: hiyo ndiyo
hekima,
nako kujitenga na uovu ndio
ufahamu.' "

*Ayubu Anamaliza Utetezi Wake*

29 [b]Ayubu akaendelea na hoja yake,
akasema:

2 [c]"Tazama jinsi ninavyoitamani miezi
iliyopita,
zile siku ambazo Mungu alikuwa
akinilinda,
3 [d]wakati taa yake iliniangazia
kichwani changu,
na kwa mwanga wake Mungu
nikapita katikati ya giza!
4 [e]Natamani siku zile nilizokuwa
katika ustawi wangu,
wakati urafiki wa Mungu wa
ndani ulipoibariki nyumba
yangu,
5 [f]wakati Mwenyezi alikuwa pamoja
nami,
nao watoto wangu walikuwa
wamenizunguka,
6 [g]wakati njia yangu ilikuwa
imenyweshewa siagi,
nao mwamba ukanimiminia vijito
vya mafuta ya zeituni.

7 [h]"Wakati nilipokwenda kwenye
lango la mji
na kuketi katika kiwanja,
8 [i]vijana waliniona wakakaa kando,
nao wazee walioketi wakasimama;
9 [j]wakuu wakaacha kuzungumza
na kuziba vinywa vyao kwa
mikono yao;
10 [k]wenye vyeo wakanyamazishwa,
nazo ndimi zao zikagandamana na
makaakaa ya vinywa vyao.
11 [l]Yeyote aliyenisikia alinena mema
juu yangu,
nao walioniona walinisifu,
12 [m]kwa sababu nilimwokoa maskini
aliyeomba msaada,
naye yatima aliyekuwa hana wa
kumsaidia.
13 [n]Mtu aliyekuwa karibu kufa
alinibariki,
nami niliufanya moyo wa mjane
kuimba.
14 [o]Niliivaa haki kama vazi langu;
uadilifu ulikuwa joho langu na
kilemba changu.
15 [p]Nilikuwa macho ya kipofu
na miguu kwa kiwete.
16 [q]Nilikuwa baba kwa mhitaji;
nilimtetea mgeni.
17 [r]Niliyavunja meno makali ya waovu,
na kuwapokonya wahanga kwenye
meno yao.

18 [s]"Nikafikiri, 'Nitafia katika nyumba
yangu mwenyewe,
nazo siku zangu zitakuwa nyingi
kama chembechembe za
mchanga.
19 [t]Mizizi yangu itafika mpaka kwenye
maji,
nao umande utakaa juu ya matawi
yangu usiku kucha.
20 [u]Utukufu wangu utabakia kuwa
mpya ndani yangu,
upinde wangu daima utaendelea
kuwa mpya mkononi
mwangu.'

[a]**28:28** Kut 20:20; Kum 4:6
[b]**29:1** Za 18:28; Ay 13:12
[c]**29:2** Yer 1:12; 44:27
[d]**29:3** Ay 11:17; 12:25
[e]**29:4** Za 25:14; Mit 3:32
[f]**29:5** Za 127:3-5; 128:3; Rum 4:1
[g]**29:6** Ay 20:17; Za 81:16; Mwa 49:20; Kum 32:13
[h]**29:7** Ay 5:4; 31:21; Yer 20:2; 38:7
[i]**29:8** 1Tim 5:1; Law 19:32
[j]**29:9** Amu 16:19; Mit 30:32
[k]**29:10** Za 137:6
[l]**29:11** Ay 4:4; Ebr 11:4
[m]**29:12** Kum 24:17; Ay 31:17-21; Za 72:12; Mit 21:13
[n]**29:13** Ay 31:20; 22:9; Kum 10:18
[o]**29:14** 2Sam 8:15; Rum 13:14; Efe 6:14
[p]**29:15** Hes 10:31
[q]**29:16** Ay 24:4; Mit 29:7
[r]**29:17** Ay 24:9; 4:10, 11; Za 3:7
[s]**29:18** Za 62:2; Mit 3:1-2
[t]**29:19** Hes 24:6; Yer 17:8
[u]**29:20** Za 18:34; Isa 38:12; Mwa 49:24

21 [a]"Watu walinisikiliza kwa tumaini,
wakingojea ushauri wangu kwa utulivu.
22 [b]Baada ya mimi kuzungumza, hawakusema zaidi;
maneno yangu yaliingia masikioni mwao kwa makini.
23 Waliningojea kama manyunyu ya mvua
na kuyapokea maneno yangu
kama ardhi inyonyavyo mvua ya vuli.
24 Walipokata tamaa niliwaonyesha uso wa furaha;
nuru ya uso wangu ilikuwa ya thamani kwao.
25 [c]Niliwachagulia njia na kukaa kama mkuu wao;
niliishi kama mfalme katikati ya majeshi yake;
nikawa kama yeye anayewafariji waombolezaji.

30 [d]"Lakini sasa watu wadogo kwa umri kuniliko wananidhihaki,
watu ambao baba zao ningekataa kwa dharau
kuwaweka pamoja na mbwa wangu wa kulinda kondoo.
2 Nguvu za mikono yao zingekuwa na faida gani kwangu,
kwa kuwa nguvu zao zilikuwa zimewaishia?
3 [e]Wakiwa wamekonda kutokana na kupungukiwa na kwa njaa,
walizurura usiku katika nchi kame iliyo ukiwa.
4 [f]Katika vichaka walikusanya mimea ya chumvi,
nacho chakula chao kilikuwa mizizi ya mti wa mfagio.
5 Walifukuzwa mbali na watu wao,
wakipigiwa kelele kama wevi.
6 [g]Walilazimika kuishi katika mikondo ya vijito vilivyokauka,
kwenye majabali na mahandaki.
7 [h]Kwenye vichaka walilia kama punda,
na walijisongasonga pamoja kwenye vichaka.
8 [i]Wao ni watoto wa wapumbavu wenye asili ya ubaya,
waliofukuzwa watoke katika nchi.

9 [j]"Nao sasa wana wao wananidhihaki katika nyimbo;
nimekuwa kitu cha dhihaka kwao.
10 [k]Wananichukia sana na kujitenga nami,
wala hawasiti kunitemea mate usoni.
11 [l]Sasa kwa kuwa Mungu ameilegeza kamba ya upinde wangu na kunitesa,
wamekuwa huru kunitendea waonavyo.
12 [m]Kuume kwangu kundi linashambulia;
wao huitegea miguu yangu tanzi,
na kunizingira.
13 [n]Huizuia njia yangu,
nao hufanikiwa katika kuniletea maafa,
nami sina yeyote wa kunisaidia.
14 Wananijia kama watu wapitao katika ufa mpana;
katikati ya magofu huja na kunishambulia.

---

[a]**29:21** Ay 29:21
[b]**29:22** Kum 32:2
[c]**29:25** Ay 31:31; 4:4
[d]**30:1** Ay 12:4; Za 119:21
[e]**30:3** Isa 8:21; Ay 24:5; Yer 17:6
[f]**30:4** Ay 39:6; 1Fal 19:4
[g]**30:6** Isa 2:19; Hos 10:8
[h]**30:7** Ay 6:5; 39:5-6
[i]**30:8** Amu 9:4; Ay 18:18
[j]**30:9** Ay 16:10; 12:4; Za 69:11; Mao 3:14; Ay 16:10; Za 69:11; Ay 12:4; Mao 3:14, 63; Ay 17:6
[k]**30:10** Hes 12:14; Mt 26:67
[l]**30:11** Mwa 12:17; Rut 1:21; Ay 41:13; Za 32:9
[m]**30:12** Za 109:6; Zek 3:1; Za 140:4-5; Ay 16:10
[n]**30:13** Isa 3:12; Za 69:26

15 [a]Vitisho vimenifunika;
heshima yangu imetoweshwa
kama kwa upepo,
salama yangu imetoweka kama
wingu.

16 [b]“Sasa maisha yangu yamefikia
mwisho;
siku za mateso zimenikamata.
17 Usiku mifupa yangu inachoma;
maumivu yanayonitafuna hayatulii
kamwe.
18 Kwa uwezo wake mkuu Mungu
huwa kwangu kama nguo;
hushikamana nami kama ukosi wa
vazi langu.
19 [c]Yeye amenitupa kwenye matope,
nami nimekuwa kama mavumbi
na majivu.

20 [d]“Ee BWANA, ninakulilia wewe lakini
hunijibu;
ninasimama, nawe unanitazama
tu.
21 [e]Wewe unanigeukia bila huruma;
unanishambulia kwa nguvu za
mkono wako.
22 [f]Unaninyakua na kunipeperusha kwa
upepo;
umenirusha huku na huko kwenye
dhoruba kali.
23 [g]Ninajua utanileta mpaka kifoni,
mahali ambapo wenye uhai wote
wamewekewa.

24 “Hakika hakuna yeyote
amshambuliaye mhitaji,
anapoomba msaada katika shida
yake.
25 [h]Je, sikulia kwa ajili ya wale
waliokuwa katika taabu?
Je, nafsi yangu haikusononeka
kwa ajili ya maskini?
26 [i]Lakini nilipotazamia mema, mabaya
yalinijia;
nilipotafuta nuru, ndipo giza
lilipokuja.
27 [j]Kusukwasukwa ndani yangu kamwe
hakutulii;
siku za mateso zinanikabili.
28 [k]Ninazunguka nikiwa nimeungua,
lakini si kwa jua;
ninasimama katika kusanyiko
nikiomba msaada.
29 [l]Nimekuwa ndugu wa mbweha,
rafiki wa mabundi.
30 [m]Ngozi yangu imekuwa nyeusi nayo
inachunika;
mifupa yangu inaungua kwa
homa.
31 [n]Kinubi changu kimegeuka kuwa
maombolezo,
nayo filimbi yangu imekuwa sauti
ya kilio.

31 [o]“Nimefanya agano na macho
yangu
yasimtazame msichana kwa
kumtamani.
2 [p]Kwa kuwa fungu la mwanadamu ni
gani kutoka kwa Mungu juu,
urithi wake kutoka kwa Mungu
Mwenye Nguvu Aliye juu?
3 [q]Je, si uharibifu kwa watu waovu,
maangamizi kwa wale watendao
mabaya?
4 [r]Je, yeye hazioni njia zangu
na kuihesabu kila hatua yangu?

5 [s]“Kama nimeishi katika uongo
au mguu wangu umekimbilia
udanganyifu,

---

[a]**30:15** Kut 3:6; Za 55:4-5; Hos 13:3; Ay 3:25
[b]**30:16** Za 22:14; Isa 53:12
[c]**30:19** Za 40:2; Yer 38:6, 22
[d]**30:20** Ay 19:7; Mao 3:8; Mt 15:23
[e]**30:21** Ay 19:6; Yer 6:23; Isa 9:12; Eze 6:14; Ay 10:3
[f]**30:22** Ay 27:21; 9:17; Yud 12
[g]**30:23** 2Sam 14:14; Ay 3:19; 10:8
[h]**30:25** Za 35:13-14; Rum 12:15; Yn 11:35
[i]**30:26** Za 82:5; Yer 8:15
[j]**30:27** Za 38:8; Mao 2:11
[k]**30:28** Mao 4:8; Za 38:6; Ay 19:7; 24:12
[l]**30:29** Isa 34:13; Yer 9:11; Za 102:6; Mik 1:8
[m]**30:30** Mao 3:4; 4:8; 5:10; Kum 28:35
[n]**30:31** Mwa 8:8; Za 137:2
[o]**31:1** Kum 5:18; Mt 5:18
[p]**31:2** Ay 16:19; 20:29
[q]**31:3** Ay 21:30; 34:22; Rum 2:9
[r]**31:4** 2Nya 16:9; Mit 5:21; Yer 32:19; Dan 4:37
[s]**31:5** Ay 15:31; Mik 2:11

6 [a]Mungu na anipime katika mizani za uaminifu,
naye atajua kwamba sina hatia:
7 [b]kama hatua zangu zimepotoka kutoka kwenye njia,
kama moyo wangu umeongozwa na macho yangu,
au kama mikono yangu imetiwa unajisi,
8 [c]basi wengine na wale nilichokipanda,
nayo yale yote niliyootesha na yang'olewe.

9 [d]"Kama moyo wangu umeshawishiwa na mwanamke,
au kama nimevizia mlangoni mwa jirani yangu,
10 [e]basi mke wangu na asage nafaka ya mwanaume mwingine,
nao wanaume wengine walale naye.
11 [f]Kwa kuwa hilo lingekuwa aibu,
naam, dhambi ya kuhukumiwa.
12 [g]Ni moto uwakao kwa Uharibifu;[h]
ungekuwa umeng'oa mavuno yangu.

13 [i]"Kama ningewanyima haki watumishi wangu wanaume au vijakazi wangu,
walipokuwa na manung'uniko dhidi yangu,
14 [j]nitafanya nini Mungu atakaponikabili?
Nitamjibu nini nitakapoitwa kutoa hesabu?
15 [k]Je, yeye aliyeniumba tumboni mwa mama yangu,
si ndiye aliwaumba?
Je, si ni yeye huyo mmoja aliyetuumba sote
ndani ya mama zetu?

16 [l]"Ikiwa nimewanyima maskini haja zao,
au kuyaacha macho ya wajane yadhoofike,
17 [m]kama nimekula chakula changu mwenyewe,
bila kuwashirikisha yatima;
18 [n]lakini tangu ujana wangu nimemlea yatima kama ambavyo baba angefanya,
nami tangu kuzaliwa kwangu nimewaongoza wajane:
19 [o]kama nilimwona yeyote akiteseka kwa kukosa nguo,
au mtu mhitaji asiye na mavazi
20 [p]ambaye wala moyo wake haukunibariki
kwa kumpatia joto kwa mavazi ya manyoya ya kondoo zangu,
21 [q]na kama nimeinua mkono wangu dhidi ya yatima,
nikijua kuwa nina ushawishi mahakamani,
22 [r]basi mkono wangu na unyofoke toka begani mwangu,
nao na uvunjike kutoka kiungio chake.
23 [s]Kwa kuwa niliogopa uharibifu kutoka kwa Mungu,
nami kwa kuuogopa utukufu wake sikuweza kufanya mambo kama hayo.

[a]**31:6** Law 19:36; Ay 6:2
[b]**31:7** Ay 9:30; Hes 15:39; Eze 6:9; Mt 5:29; Mhu 11:9
[c]**31:8** Law 26:16; Yn 4:37; Mik 6:15
[d]**31:9** Kum 11:16; Yak 1:14
[e]**31:10** Kum 28:30; Yer 8:16; Mit 14:31
[f]**31:11** Law 20:10; Yn 8:4-5
[g]**31:12** Ay 15:30; 26:6
[h]12 Kwa Kiebrania ni Abadon (Ay 26:6; Mit 15:11).
[i]**31:13** Kut 21:2-11; Law 25:39-46
[j]**31:14** Ay 33:5; Hos 9:7; Za 10:13, 15; Isa 10:3; Yer 5:31
[k]**31:15** Ay 10:3; Efe 6:9
[l]**31:16** Law 25:17; Ay 20:19; Yak 1:27
[m]**31:17** Ay 6:27; 29:12
[n]**31:18** Isa 51:18
[o]**31:19** Ay 22:6; 24:4; Isa 58:7
[p]**31:20** Ay 29:13; Amu 6:37
[q]**31:21** Ay 22:7-9; Yak 1:27
[r]**31:22** Hes 15:30; Za 10:15
[s]**31:23** Ay 10:3; 13:11; Mwa 20:11

24 [a]"Kama nimeweka tumaini langu
kwenye dhahabu,
au kuiambia dhahabu safi, 'Wewe
ndiwe salama yangu,'
25 [b]kama nimefurahia wingi wa utajiri
wangu,
ustawi ambao mikono yangu
ilikuwa imepata,
26 [c]kama nimelitazama jua katika
kung'aa kwake
au mwezi ukienda kwa fahari
yake,
27 [d]hivyo moyo wangu kushawishiwa
kwa siri,
au kubusu mkono wangu kwa
kuviheshimu,
28 [e]basi hiyo pia ingekuwa dhambi ya
kuhukumiwa,
kwa kuwa ningekuwa si
mwaminifu kwa Mungu
aishiye juu sana.

29 [f]"Kama nimeshangilia msiba wa adui
yangu,
au kutazama kwa furaha taabu
iliyomjia,
30 lakini sikuruhusu kinywa changu
kufanya dhambi
kwa kuomba laana dhidi ya
maisha yake;
31 kama watu wa nyumbani mwangu
kamwe hawakusema,
'Ni nani ambaye hajashibishwa na
nyama ya Ayubu?'
32 [g]Lakini hakuna mgeni aliyelala
njiani,
kwa maana mlango wangu
ulikuwa wazi kwa msafiri;
33 [h]kama nimeifunika dhambi yangu
kama wanadamu wengine
wafanyavyo,
kwa kuficha hatia yangu moyoni
mwangu,
34 [i]kwa sababu ya kuogopa umati wa
watu,
na hivyo kuwa na hofu ya
kudharauliwa na jamaa,
nikanyamaza kimya nisitoke nje
ya mlango:

35 ("Laiti kama angekuwepo mtu wa
kunisikia!
Tazama sasa ninatia sahihi kwenye
utetezi wangu:
Mwenyezi na anijibu;
mshtaki wangu na aweke mashtaka
yake kwenye maandishi.
36 Hakika ningeyavaa begani mwangu,
ningeyavaa kama taji.
37 [j]Ningempa hesabu ya kila hatua
yangu,
ningemwendea kama mwana wa
mfalme.)

38 [k]"Kama nchi yangu inalia dhidi
yangu,
na mifereji yake yote imelowana
kwa machozi,
39 [l]kama nimekula mazao yake bila
malipo,
au kuvunja mioyo ya wapangaji
wake,
40 [m]basi miiba na iote badala ya ngano,
na magugu badala ya shayiri."

Mwisho wa maneno ya Ayubu.

## SEHEMU YA TATU: MAZUNGUMZO YA ELIHU

*(Ayubu 32–37)*

### *Elihu Awakemea Rafiki Za Ayubu*

1 [n]Basi watu hawa watatu wakaacha
kumjibu Ayubu, kwa kuwa alikuwa
mwadilifu machoni pake mwenyewe.

[a]**31:24** Ay 22:25; Mk 10:24; Lk 12:15
[b]**31:25** Mwa 12:16; Isa 10:14
[c]**31:26** Hes 11:20; Kum 4:19; Eze 8:16
[d]**31:27** Ay 24:15; Yak 1:14; Yer 8:2; 16:11
[e]**31:28** Mwa 38:24; Kum 17:2-7; Yos 24:23-27; Mit 30:9
[f]**31:29** Za 35:15; Mt 5:44; Mit 17:5; 24:17-18
[g]**31:32** Amu 19:20; Mt 25:35; Ebr 13:2; 1Pet 4:9
[h]**31:33** Za 32:5; Mit 28:13; Mwa 3:8
[i]**31:34** Kut 23:2; Mit 29:25
[j]**31:37** Ay 1:3; 21:28
[k]**31:38** Mwa 4:10
[l]**31:39** 1Fal 21:19; Law 19:13; Yak 5:4
[m]**31:40** Mwa 3:18; Mit 13:7
[n]**32:1** Ay 2:3; 10:7

2 [a]Lakini Elihu mwana wa Barakeli,
wa kabila la Buzi wa jamaa ya Ramu,
akamkasirikia sana Ayubu, kwa sababu
ya kujihesabia haki mwenyewe badala
ya Mungu. 3 [b]Pia aliwakasirikia hao rafiki
watatu wa Ayubu, kwa sababu hawakuweza
kupata njia ya kuthibitisha ya kuwa hayo
maneno ya Ayubu hayakuwa ya kweli,
nao bado walikuwa wamemlaumu. 4 [c]Basi
Elihu alikuwa amesubiri kwanza waongee
na Ayubu kwa sababu walikuwa na umri
mkubwa kumliko yeye. 5 Lakini alipoona
watu hao watatu hawakuwa na kitu zaidi
cha kusema, hasira yake ikaamka.

6 [d]Basi Elihu mwana wa Barakeli wa
kabila la Buzi akasema:

"Mimi ni mdogo kwa umri,
nanyi ni wazee;
ndiyo sababu niliogopa,
sikuthubutu kuwaambia kile
ninachojua.
7 [e]Nilifikiri, 'Yafaa umri useme,
nao wingi wa miaka ungefundisha
hekima.'
8 [f]Lakini ni Roho iliyoko ndani ya
mwanadamu,
pumzi ya Mwenyezi, ndiyo impayo
yeye ufahamu.
9 [g]Sio wazee peke yao walio na
hekima,
sio wenye umri mkubwa peke yao
wanaofahamu lililo sawa.

10 [h]"Kwa hiyo nasema: Nisikilizeni
mimi;
mimi nami nitawaambia lile
ninalojua.
11 Nilingojea mlipokuwa mnaongea,
nilizisikiliza hoja zenu;
mlipokuwa mkitafuta maneno ya
kusema,
12 [i]niliwasikiliza kwa makini.
Lakini hakuna hata mmoja wenu
aliyethibitisha kwamba Ayubu
amekosa;
hakuna hata mmoja wenu
aliyeweza kujibu hoja zake.
13 [j]Msiseme, 'Tumepata hekima;
Mungu na amthibitishe kuwa
mwongo,
wala si mwanadamu.'
14 [k]Lakini Ayubu hajayapanga maneno
yake dhidi yangu,
nami sitamjibu kwa kutumia hoja
zenu.

15 [l]"Wametiwa hofu na hawana la zaidi
la kusema;
maneno yamewaishia.
16 Je, ningoje sasa kwa sababu
wamekuwa kimya,
kwa vile sasa wanasimama bila
kuwa na la kujibu?
17 [m]Mimi nami nitakuwa na la kusema;
mimi nami nitasema lile nilijualo.
18 [n]Kwa kuwa nimejawa na maneno,
nayo Roho iliyomo ndani yangu
yanisukuma;
19 [o]ndani yangu niko kama chupa
iliyojazwa divai,
kama kiriba kipya cha divai
kilicho tayari kupasuka.
20 [p]Ni lazima niseme ili niweze kutulia;
ni lazima nifumbue midomo yangu
nipate kujibu.
21 [q]Sitampendelea mtu yeyote,
wala sitajipendekeza kwa mtu
yeyote;

---

[a]**32:2** Mwa 22:21; Ay 13:19; 35:2
[b]**32:3** Ay 42:7; 32:12-13; 15:13
[c]**32:4** Law 19:32
[d]**32:6** Ay 15:10
[e]**32:7** 1Nya 29:15; 2Nya 10:6
[f]**32:8** Ay 27:3; 33:4; Mit 2:6; 1Fal 3:9
[g]**32:9** 1Kor 1:21-26
[h]**32:10** Ay 33:1; 31:33; Za 34:11; Ay 5:27
[i]**32:12** Ay 32:3
[j]**32:13** Mhu 9:11; Yer 9:23
[k]**32:14** Ay 23:4
[l]**32:15** Ay 32:1
[m]**32:17** Ay 5:27; 33:3; 36:4
[n]**32:18** Mdo 4:20; 1Kor 9:16; 2Kor 5:14
[o]**32:19** Yer 20:9; Amo 3:8; Mt 9:17
[p]**32:20** Ay 4:2; Yer 6:11
[q]**32:21** Law 19:15; 2Nya 19:7; Mt 22:16

22 [a]kwa kuwa kama ningekuwa stadi wa
kujipendekeza,
Muumba wangu angeniondolea
mbali kwa upesi.

*Elihu Anamkemea Ayubu*

33 [b]“Lakini Ayubu, sasa, sikiliza
maneno yangu;
zingatia kila kitu nitakachosema.
2 Karibu nitafungua kinywa changu;
maneno yangu yapo katika ncha
ya ulimi wangu.
3 [c]Maneno yangu yanatoka katika
moyo mnyofu;
midomo yangu hunena kwa
uaminifu yale niyajuayo.
4 [d]Roho wa Mungu ameniumba;
pumzi ya Mwenyezi hunipa uhai.
5 [e]Unijibu basi, kama unaweza;
jiandae kunikabili mimi.
6 [f]Mimi ni kama wewe mbele za
Mungu;
mimi pia nimetolewa kwenye
udongo.
7 [g]Huna sababu ya kuniogopa,
wala mkono wangu haupaswi
kukulemea.

8 “Lakini umesema nikiwa
ninakusikia,
nami nilisikia maneno yenyewe:
9 [h]‘Mimi ni safi na sina dhambi;
mimi ni safi na sina hatia.
10 [i]Lakini bado Mungu amepata dosari
kwangu,
naye ananiona kama adui yake.
11 [j]Ananifunga miguu kwa pingu,
tena anaziangalia njia zangu zote
kwa karibu.’

12 [k]“Lakini mimi ninakuambia, katika
jambo hili wewe una makosa,
kwa maana Mungu ni mkuu kuliko
mwanadamu.
13 [l]Kwa nini unamlalamikia
kwamba yeye hamjibu
mwanadamu?
14 [m]Kwa kuwa Mungu husema, wakati
huu kwa njia moja,
au wakati mwingine kwa njia
nyingine,
ingawa mwanadamu anaweza
asielewe.
15 [n]Mungu husema na mwanadamu
katika ndoto,
katika maono ya usiku,
wakati usingizi mzito uwaangukiapo
wanadamu wasinziapo vitandani
mwao,
16 [o]anaweza akasemea masikioni mwao,
na kuwatia hofu kwa maonyo,
17 [p]ili kumgeuza mtu kutoka kwenye
kutenda mabaya
na kumwepusha na kiburi,
18 [q]kuiokoa nafsi yake na shimo,
uhai wake usiangamizwe kwa
upanga.
19 [r]Mtu anaweza kutiwa adabu kwa
maumivu kitandani mwake,
kwa dhiki za mfululizo katika
mifupa yake,
20 [s]kiasi kwamba maisha yake yenyewe
yanakataa chakula
nayo nafsi yake ikakichukia kabisa
hata chakula kizuri.
21 [t]Nyama ya mwili wake huisha kwa
kukonda,
nayo mifupa yake ambayo
mwanzoni ilikuwa imefichika,
sasa inatokeza nje.

---

[a]**32:22** Ay 4:17; 9:9; Za 12:2-4
[b]**33:1** Ay 32:10; 6:28; 13:6
[c]**33:3** Ay 27:4; 36:4
[d]**33:4** Mwa 2:7; Ay 10:3; 27:3
[e]**33:5** Ay 13:18
[f]**33:6** Ay 9:32; 4:19
[g]**33:7** Ay 13:21; 2Kor 2:4
[h]**33:9** Ay 10:7; 9:30; 16:17
[i]**33:10** Ay 13:24
[j]**33:11** Ay 13:27; Mit 3:6; Isa 30:21
[k]**33:12** Mhu 7:20; Za 8:4; Isa 55:8-9
[l]**33:13** Ay 40:2; Isa 45:9
[m]**33:14** Za 62:11; Mwa 30:2; Mt 27:19
[n]**33:15** Mwa 30:2; Mt 27:19
[o]**33:16** Ay 36:10
[p]**33:17** Ay 36:10, 15; 6:4; Za 88:15-16
[q]**33:18** Yn 2:6; Zek 9:11; Ay 15:22; Mt 26:52
[r]**33:19** Kum 8:5; Za 6:2; Isa 38:13
[s]**33:20** Za 102; 4; 107:18; Ay 3:24
[t]**33:21** Ay 2:5; 16:8

22 [a]Nafsi yake inakaribia kaburi,
nao uhai wake karibu na wajumbe
wa kifo.

23 [b]“Kama bado kuna malaika upande
wake
kama mtetezi, mmoja miongoni
mwa elfu,
wa kumwambia mwanadamu lililo
jema kwake,
24 [c]kumwonea huruma na kusema,
‘Mwokoe asije akatumbukia
shimoni;
nimepata ukombozi kwa ajili
yake’:
25 [d]ndipo nyama ya mwili wake
hufanywa mpya kama ya
mtoto;
hurudishwa upya kama siku za
ujana wake.
26 [e]Humwomba Mungu, akapata kibali
kwake,
huuona uso wa Mungu na
kushangilia kwa furaha;
Mungu humrudisha katika hali
yake ya uadilifu.
27 [f]Ndipo huja mbele za watu na
kusema,
‘Nilitenda dhambi na kupotosha
kilichokuwa haki,
lakini sikuadhibiwa kama
nilivyostahili.
28 [g]Alinikomboa nafsi yangu
nisitumbukie shimoni,
nami nitaishi ili kuufurahia
mwanga.’

29 [h]“Mungu hufanya haya yote kwa
mwanadamu;
mara mbili hata mara tatu,
30 [i]ili aigeuze nafsi yake toka shimoni,
ili nuru ya uzima imwangazie.

31 [j]“Ayubu, zingatia, nisikilize mimi;
nyamaza, nami nitanena.
32 [k]Kama unalo lolote la kusema,
unijibu;
sema, kwa maana ninataka
uonekane huna hatia.
33 [l]Lakini kama huna la kusema, basi
nisikilize mimi;
nyamaza, nami nitakufundisha
hekima.”

*Elihu Anatangaza Haki Ya Mungu*

34 Kisha Elihu akasema:

2 [m]“Sikieni maneno
yangu, enyi watu wenye
hekima;
nisikilizeni mimi, ninyi watu
wenye maarifa.
3 [n]Kwa kuwa sikio huyajaribu maneno
kama vile ulimi uonjavyo chakula.
4 [o]Tujichagulie wenyewe yaliyo sawa,
nasi tujifunze pamoja yaliyo
mema.

5 [p]“Ayubu anasema, ‘Mimi sina hatia,
lakini Mungu ameninyima haki
yangu.
6 [q]Ingawa niko sawa,
ninaonekana mwongo;
nami ingawa sina kosa,
kidonda changu hakiponi.’
7 [r]Ni mtu gani aliye kama Ayubu,
anywaye dharau kama maji?
8 [s]Ashirikianaye na watenda mabaya
na kuchangamana na watu waovu.

[a]**33:22** Ay 38:17; Za 9:13; 88:3; 107:18; 116:3
[b]**33:23** Ay 36:9-10; Mik 6:8; Gal 3:19; Ebr 8:6; 9:15; Ay 36:9-10; Mik 6:8
[c]**33:24** Isa 38:17
[d]**33:25** 2Fal 5:14
[e]**33:26** Mit 8:35; 2Fal 20:2-5; Lk 2:52; Ezr 3:13; Za 13:5
[f]**33:27** Hes 22:34; 2Sam 12:13; Ezr 9:13; Yak 2:13; Lk 15:21
[g]**33:28** Kut 15:13; Za 34:22; 107:20; Ay 17:16; 22:20
[h]**33:29** Yer 10:23; Flp 2:13
[i]**33:30** Za 49:19; Isa 53:11; Zek 9:11
[j]**33:31** Yer 23:18; Ay 32:10
[k]**33:32** Ay 6:29; 35:2
[l]**33:33** Mit 10:8, 10, 19; Za 34:11
[m]**34:2** Ay 32:10
[n]**34:3** Ay 12:11
[o]**34:4** 1The 5:21
[p]**34:5** Ay 33:9; 6:29; 27:2; 9; 17
[q]**34:6** Yer 10:19; Ay 10:3
[r]**34:7** Ay 9:21; 15:16
[s]**34:8** Ay 22:15; Za 50:18

9 [a]Kwa kuwa anasema, 'Haimfaidi
mwanadamu kitu chochote
anapojitahidi kumpendeza
Mungu.'

10 [b]"Hivyo nisikilizeni mimi, ninyi watu
wenye ufahamu.
Kamwe Mungu hatendi uovu,
Mwenyezi hafanyi kosa.
11 [c]Humlipa mwanadamu kwa ajili ya
lile alilotenda;
huleta juu yake kile ambacho
matendo yake yanastahili.
12 [d]Ni jambo lisiloweza kufikiriwa
kwamba Mungu angefanya
makosa,
kwamba Mwenyezi angepotosha
hukumu.
13 [e]Je, ni nani aliyemtawaza juu ya
dunia?
Ni nani aliyemweka kuwa
mwangalizi wa ulimwengu
wote?
14 [f]Kama lilikuwa kusudi la Mungu,
naye akaiondoa Roho yake na
pumzi yake,
15 [g]wanadamu wote wangeliangamia
kwa pamoja,
na mtu angerudi mavumbini.

16 [h]"Kama ninyi mnaufahamu, sikieni
hili;
sikilizeni hili nisemalo.
17 [i]Je, yeye aichukiaye haki aweza
kutawala?
Je, utamhukumu mwenye haki,
Aliye na Nguvu Zote?
18 [j]Je, si ni yeye awaambiaye wafalme,
'Ninyi hamfai kitu,'
nao watu mashuhuri, 'Ninyi ni
waovu,'
19 [k]yeye asiyependelea wakuu,
wala haonyeshi upendeleo kwa
matajiri kuliko maskini,
kwa kuwa wote ni kazi ya mikono
yake?
20 [l]Wanakufa ghafula, usiku wa
manane;
watu wanatikiswa nao hupita;
wenye nguvu huondolewa
bila mkono wa mwanadamu.

21 [m]"Macho yake yanazitazama njia za
wanadamu;
anaona kila hatua yao.
22 [n]Hakuna mahali penye giza nene,
wala uvuli mkubwa,
ambapo watenda mabaya
wanaweza kujificha.
23 [o]Mungu hana haja ya kumchunguza
mtu sana,
ili apate kuja mbele zake kwa
hukumu.
24 [p]Bila kuuliza huwapondaponda
wenye nguvu nyingi
na kuwaweka wengine mahali
pao.
25 [q]Kwa sababu huyaangalia matendo
yao yote,
huwaondoa usiku, nao
wakaangamia.
26 [r]Anawaadhibu kwa ajili ya uovu wao
mahali ambapo kila mmoja
ataweza kuwaona,

---

[a]**34:9** Ay 9:29-31
[b]**34:10** Mwa 18:25; Za 92:15; Rum 3:5
[c]**34:11** Ay 21:31; 2Kor 5:10; Yer 17:10; Eze 33; 20; Mit 24:12
[d]**34:12** Za 9:16; Kol 3:25
[e]**34:13** Ay 36:23; Isa 40:14
[f]**34:14** Hes 16:22; Za 104:29; Mhu 12:7
[g]**34:15** Za 90:10; Mwa 2:7
[h]**34:16** Ay 32:10; 34:30
[i]**34:17** Mwa 18:23; 2Sam 23:3-4; Mit 20:8; Rum 3:5-7; Ay 10:7
[j]**34:18** Kut 22:28; Isa 40:24
[k]**34:19** Kum 10:17; Mdo 10:34; Law 19:15; Yak 2:5
[l]**34:20** Kut 11:4; 12:29; Ay 12:19
[m]**34:21** Mit 15:3; Ebr 4:13
[n]**34:22** Za 74:20; Ay 3:5; Amo 9:2-3
[o]**34:23** Ay 11:11; Ezr 9:13
[p]**34:24** Ay 12:19; Dan 2:21
[q]**34:25** Ay 11:11; Mit 5:21-23
[r]**34:26** Mwa 6:5; Ay 8:22; 28:24; Za 9:5; Yer 44:5

27 [a]kwa sababu wameacha kumfuata
Mungu,
nao hawakuiheshimu njia yake
hata moja.
28 [b]Wamesababisha kilio cha maskini
kifike mbele zake,
hivyo akasikia kilio cha wahitaji.
29 [c]Lakini kama akinyamaza kimya,
ni nani awezaye kumhukumu?
Kama akiuficha uso wake,
ni nani awezaye kumwona?
Ikiwa ni taifa au mtu mmoja, kwake
ni sawa,
30 [d]ili kumzuia mtu mwovu kutawala,
au wale ambao huwategea watu
mitego.

31 "Kama mwanadamu akimwambia
Mungu,
'Nimekosa lakini sitatenda dhambi
tena.
32 [e]Nifundishe nisichoweza kuona;
kama nimekukosea, sitafanya
hivyo tena.'
33 [f]Je basi, Mungu atakulipa kwa
masharti yako,
wakati wewe umekataa kutubu?
Yakupasa wewe uamue, wala si
mimi;
sasa niambie lile ulijualo.

34 "Wanadamu wenye ufahamu
husema,
wenye hekima wanaonisikia
huniambia,
35 [g]'Ayubu huongea bila maarifa;
maneno yake hayana busara.'
36 [h]Laiti Ayubu angejaribiwa hadi
kikomo cha mwisho,
kwa sababu anajibu kama mtu
mwovu!
37 Kwenye dhambi yake huongeza uasi;
kwa dharau hupiga makofi
miongoni mwetu,
na kuzidisha maneno yake dhidi
ya Mungu."

*Elihu Analaumu Mtu Kujiona Kuwa Mwenye Haki*

35 Ndipo Elihu akasema:
2 [i]"Je, unadhani hili ni
haki?
Wewe unasema, 'Nina haki mbele
za Mungu.'
3 [j]Bado unamuuliza, 'Ni faida gani
nimepata,
na imenifaidi nini kwa
kutokutenda dhambi?'

4 "Ningependa nikujibu wewe
pamoja na marafiki zako walio
pamoja nawe.
5 [k]Tazama juu mbinguni ukaone;
yaangalie mawingu yaliyo juu
sana juu yako.
6 [l]Je, ukitenda dhambi, inamdhuruje
Mungu?
Kama dhambi zako zikiwa nyingi,
hilo linamfanyia nini Mungu?
7 [m]Kama wewe ni mwadilifu, unampa
nini,
au yeye anapokea nini mkononi
kwako?
8 [n]Uovu wako unamdhuru tu mtu
mwingine kama wewe,
nayo haki yako inawafaa
wanadamu tu.

9 [o]"Wanadamu hulia kwa kulemewa
na mateso;
huomba msaada kutoka mkono
wenye nguvu.

---

[a]**34:27** Za 14:3; Isa 5:12; 1Sam 15:11
[b]**34:28** Kut 22:23; Yak 5:4; Mhu 5:8
[c]**34:29** Za 28:1; 83:1; 109:1; Rum 8:34; Za 13:1; 97:9; 83:18
[d]**34:30** Za 25:15; Mit 29:2-12; 1Fal 12:28-30
[e]**34:32** Kut 33:13; Za 27:11; Lk 19:8; Ay 33:27
[f]**34:33** Mit 17:23; Yn 3:8
[g]**34:35** Ay 35:16; 38:2; 42:3; 26:3
[h]**34:36** Ay 6:29; 22:15
[i]**35:2** Ay 33:32; 2:9; 32:2
[j]**35:3** Ay 21:15; 34:9
[k]**35:5** Kum 10:14; Mwa 15:5; Ay 22:12; Za 19:1-4
[l]**35:6** Ay 7:20; Mit 8:36
[m]**35:7** Rum 11:35; Mit 9:12; 1Kor 4:7; Lk 17:10
[n]**35:8** Eze 18:24; 18:5-9; Zek 7:9-10
[o]**35:9** Kut 2:23; Ay 5:15; 12:19; Lk 18:3-7

[10] [a]Lakini hakuna asemaye, ‘Yuko wapi
Mungu Muumba wangu,
yeye anifanyaye niimbe usiku,
[11] [b]yeye atufundishaye sisi zaidi kuliko
wanyama wa dunia,
na kutufanya wenye hekima
kuliko ndege wa angani?’
[12] [c]Yeye hajibu wakati watu waliapo
kwa sababu ya kiburi cha watu
waovu.
[13] [d]Naam, Mungu hasikilizi maombi
yao ya ubatili;
Mwenyezi hayazingatii.
[14] [e]Si zaidi sana kwamba hatakusikiliza
wewe usemapo humwoni,
tena ya kwamba shauri lako liko
mbele zake
na wewe lazima umngojee,
[15] pia zaidi, kwamba hasira yake
kamwe haiadhibu
wala haangalii uovu hata kidogo?
[16] [f]Hivyo Ayubu hufumbua kinywa
chake kwa maneno yasiyo na
maana;
anaongea maneno mengi bila
maarifa.”

*Elihu Atukuza Wema Wa Mungu*

36 Elihu akaendelea kusema:

[2] “Nivumilie kidogo
zaidi nami nitakuonyesha
kwamba yako mengi zaidi ya
kusemwa kwa ajili ya Mungu.
[3] [g]Ninayapata maarifa yangu kutoka
mbali,
nami nitamhesabia haki Muumba
wangu.
[4] [h]Uwe na hakika kwamba maneno
yangu si ya uongo;
mmoja aliye mkamilifu katika
maarifa yuko pamoja na
wewe.

[5] [i]“Mungu ni mwenye nguvu, lakini
hamdharau mwanadamu;
ni mwenye nguvu, naye ni thabiti
katika shauri lake.
[6] [j]Hawaachi waovu waendelee kuishi,
bali huwapa walioteswa haki yao.
[7] [k]Yeye haondoi macho yake kwa
wenye haki;
huwaketisha penye viti vya enzi
pamoja na wafalme
na kuwatukuza milele.
[8] [l]Lakini ikiwa watu wamefungwa
kwenye minyororo,
wakiwa wameshikiliwa na kamba
za mateso,
[9] [m]huwaonyesha yale waliyoyatenda,
kwamba wametenda dhambi kwa
majivuno.
[10] [n]Huwafanya wao kusikia maonyo,
na huwaagiza kutubu uovu wao.
[11] [o]Kama wakitii na kumtumikia,
wataishi siku zao zilizobaki katika
mafanikio,
na miaka yao katika utoshelevu.
[12] [p]Lakini wasiposikiliza,
wataangamia kwa upanga,
nao watakufa pasipo maarifa.

[13] [q]“Wasiomcha Mungu moyoni mwao
huficha chuki;
hata anapowafunga, hawamwombi
msaada.
[14] [r]Wanakufa wangali vijana,
miongoni mwa wanaume hanithi
wa mahali pa kuabudia
miungu.

---

[a]**35:10** Ay 4:17; Isa 51:13; Za 77:6; Mdo 16:25; 1Pet 4:19
[b]**35:11** Za 94:12; Lk 12:24; Ay 32:8
[c]**35:12** 1Sam 8:18; Mit 1:1
[d]**35:13** Kum 1:45; 1Sam 8:18; Ay 15:31; Mit 15:8
[e]**35:14** Ay 9:11; Yer 11:11
[f]**35:16** Ay 34:35-37; 1Kor 4:20
[g]**36:3** Ay 4:17; 8:3
[h]**36:4** Ay 6:28; 13:6; 37:5, 16, 23; 32:17
[i]**36:5** Za 31:22; 69:33; Hes 23:19; Rum 11:29
[j]**36:6** Ay 8:22; 4:10
[k]**36:7** Za 34:15; 113:8; Mt 6:18; Isa 22:23
[l]**36:8** 2Sam 3:34; 2Fal 23:33
[m]**36:9** Ay 15:25
[n]**36:10** Ay 33:16; 2Fal 17:13; Ay 5:17
[o]**36:11** Kut 28:1; Hag 1:12; Isa 1; 19
[p]**36:12** Law 26:38; Ay 15:22; 4:21; Efe 4:18
[q]**36:13** Ay 15:12; Rum 2:5; Ay 5:2; 4:17; Amo 4:11
[r]**36:14** Kum 23:17

15 [a]Bali wao wanaoteseka huwaokoa
katika mateso yao,
na kuzungumza nao katika dhiki
zao.

16 [b]"Yeye anakubembeleza utoke katika
mataya ya dhiki,
ili kukuweka mahali palipo na
nafasi mbali na kizuizi,
hadi kwenye meza yako ya faraja
iliyojaa vyakula vizuri.
17 [c]Lakini sasa umelemewa na hukumu
kwa ajili ya uovu;
hukumu na haki vimekukamata.
18 [d]Uwe mwangalifu ili yeyote
asikushawishi kwa utajiri;
usipotoshwe kwa fungu kubwa la
rushwa.
19 [e]Je, utajiri wako hata nguvu zako
nyingi
vinaweza kukusaidia usiingie
kwenye dhiki?
20 [f]Usiutamani usiku uje,
ili uwaburute watu mbali na
nyumba zao.
21 [g]Jihadhari usigeukie uovu,
ambao unaupenda zaidi kuliko
mateso.

22 [h]"Mungu ametukuzwa katika nguvu
zake.
Ni nani aliye mwalimu kama
yeye?
23 [i]Ni nani aliyemwelekeza katika njia
zake,
au kumwambia, 'Wewe umetenda
yasiyo sawa'?
24 [j]Kumbuka kuzitukuza kazi zake,
ambazo watu wamezisifu katika
wimbo.
25 [k]Wanadamu wote wameiona;
watu wanaikazia macho kwa
mbali.
26 [l]Tazama jinsi Mungu alivyo mkuu,
kupita ufahamu wetu!
Hesabu ya miaka yake haitafutiki.

27 [m]"Yeye huvuta juu matone ya maji,
ayachujayo kama mvua kutoka
kwenye vijito;
28 [n]mawingu huangusha chini maji
yake,
nayo mvua nyingi huwanyeshea
wanadamu.
29 [o]Ni nani ajuaye jinsi ayatandazavyo
mawingu,
jinsi angurumavyo kutoka hemani
mwake.
30 [p]Tazama jinsi anavyotandaza umeme
wa radi kumzunguka,
naye huvifunika vilindi vya
bahari.
31 [q]Hivi ndivyo atawalavyo mataifa,
na kuwapa chakula kwa wingi.
32 [r]Huujaza mkono wake kwa umeme
wa radi,
na kuuagiza kulenga shabaha
yake.
33 Ngurumo zake hutangaza dhoruba
inayokuja;
hata mifugo hujulisha kukaribia
kwake.[s]

37 [t]"Kwa hili moyo wangu
unatetemeka,
nao unaruka kutoka mahali pake.

[a]**36:15** Ay 5:15; 2Kor 12:10; Ay 33:16; 34:33
[b]**36:16** Hos 2:14; Za 23:5; 78:19
[c]**36:17** Ay 20:29; 22:11
[d]**36:18** Kut 23:8; Amo 5:12; Ay 34:33
[e]**36:19** Za 49:6; Yer 9:23
[f]**36:20** Ay 34:20-25
[g]**36:21** Ay 34:33; Za 66:18; Ebr 11:25
[h]**36:22** Isa 40:13; Rum 11:34
[i]**36:23** Ay 34:10, 13; Rum 11:33; Mwa 18:25; Kum 32:4
[j]**36:24** 1Nya 16:24; Za 35:27; 59:16; Ufu 15:3
[k]**36:25** Rum 1:20
[l]**36:26** 1Kor 13:12; Mwa 21:33; Ebr 1:12
[m]**36:27** 2Sam 1:21; Za 147:8
[n]**36:28** Ay 22:11; Mt 5:45
[o]**36:29** Mit 8:28; Isa 40:22
[p]**36:30** Kut 19:16; Yer 10:13; Hab 3:11; Isa 51:10; Za 18:12, 14; 97:4
[q]**36:31** 1Fal 17:1; Amo 4:7-8; Isa 30:23; Mdo 14:17
[r]**36:32** Ay 28:24; Za 18:14
[s]33 Au: hutangaza kuja kwake.
[t]**37:1** Za 38:10; Isa 15:5; Yer 4:19; Hab 3:16

2 [a]Sikiliza! Sikiliza ngurumo ya sauti yake,
sauti ya ngurumo itokayo kinywani mwake.
3 [b]Huuachilia umeme wake wa radi chini ya mbingu yote
na kuupeleka hata miisho ya dunia.
4 [c]Baada ya hayo huja sauti ya ngurumo yake;
Mungu hunguruma kwa sauti yake ya fahari.
Wakati sauti yake ingurumapo tena,
huuachilia umeme wake wa radi.
5 [d]Sauti ya Mungu hunguruma kwa namna za ajabu;
yeye hutenda mambo makuu kupita ufahamu wetu.
6 [e]Huiambia theluji, ‘Anguka juu ya dunia,’
nayo manyunyu ya mvua, ‘Uwe mvua ya nguvu.’
7 [f]Ili wanadamu wote aliowaumba wapate kujua kazi zake,
yeye humzuilia kila mtu shughuli zake.
8 [g]Wanyama hujificha;
hubakia kwenye mapango yao.
9 [h]Dhoruba hutoka katika chumba chake,
baridi hutoka katika upepo uendao kasi.
10 [i]Pumzi ya Mungu hutoa barafu,
eneo kubwa la maji huganda.
11 [j]Huyasheheneza mawingu kwa maji,
naye husambaza umeme wake wa radi kupitia hayo.
12 [k]Nayo mawingu huzungukazunguka pande zote kwa amri yake,
juu ya uso wa dunia yote,
kufanya lolote ayaamuruyo.
13 [l]Huleta mawingu ili kuadhibu wanadamu,
au kuinyeshea dunia yake na kuonyesha upendo wake.

14 [m]“Ayubu, sikiliza hili;
nyamaza na uyafikiri maajabu ya Mungu.
15 [n]Je, unajua jinsi Mungu anavyoyaongoza mawingu,
na kufanya umeme wake wa radi utoe mwanga?
16 [o]Je, wajua jinsi mawingu yanavyokaa yakiwa yametulia,
hayo maajabu yake yeye aliye mkamilifu katika maarifa?
17 [p]Wewe unayeshindwa na joto katika nguo zako
wakati nchi imenyamazishwa kimya bila upepo wa kusini,
18 [q]je, waweza kuungana naye katika kuzitandaza anga,
zilizo ngumu kama kioo cha shaba ya kuyeyushwa?

19 [r]“Tuambieni yatupasayo kumwambia;
hatuwezi kutayarisha shauri letu kwa sababu ya ujinga wetu.
20 Je, aambiwe kwamba nataka kuongea?
Je, yuko mtu ambaye angeomba kumezwa?
21 [s]Basi hakuna awezaye kulitazama jua,
jinsi linavyong’aa angani,
upepo ukishafagia mawingu.

---

[a]**37:2** Za 18:13; 29:3-9
[b]**37:3** 2Sam 22:13; Za 18:14; Ay 36:32; Mt 24:27; Lk 17:24
[c]**37:4** 1Sam 2:10; Kut 20:19
[d]**37:5** Ay 11:7-9
[e]**37:6** Kum 28:12; Ay 38:22; Mwa 7:4; Ay 36:27
[f]**37:7** Ay 12:14; Za 111:2; 109:27; 104:19-23
[g]**37:8** Ay 28:26; 38:40; Za 104:22
[h]**37:9** Za 50:3; 147:17
[i]**37:10** Ay 38:29-30; Za 147:17
[j]**37:11** Ay 26:8; 36:30; 28:26
[k]**37:12** Za 147:16; 148:8; Ay 37:3
[l]**37:13** Kut 9:22-23; 1Sam 12:17; Kut 9:18; 1Fal 18:45
[m]**37:14** Ay 32:10; 5:9
[n]**37:15** Ay 36:30, 32
[o]**37:16** Ay 36:29; 5:9; 36:4
[p]**37:17** Mdo 27:13
[q]**37:18** Mwa 1:1, 8; Ay 22:14; Kum 28:23; Za 104:2
[r]**37:19** Rum 8:26; Ay 13:18; 9:3
[s]**37:21** Amu 5:31; Mdo 22:1; 26:13

22 [a]Kutoka kaskazini yeye huja na fahari
kuu;
Mungu huja katika utukufu wa
kutisha.
23 [b]Yeye Mwenyezi hatuwezi kumfikia,
naye ametukuzwa katika
uweza;
katika hukumu zake na haki yake
kuu, hataonea.
24 [c]Kwa hiyo, wanadamu mheshimuni,
kwa kuwa yeye hamstahi yeyote
anayejidhania kuwa ana
hekima."

## SEHEMU YA NNE: MUNGU ANAZUNGUMZA

*(Ayubu 38–41)*

*Bwana Anamjibu Ayubu*

1 [d]Kisha Bwana akamjibu Ayubu kutoka
upepo wa kisulisuli. Akasema:

2 [e]"Nani huyu atiaye mashauri yangu
giza
kwa maneno yasiyo na maarifa?
3 [f]Jikaze kama mwanaume;
nitakuuliza swali,
nawe unijibu.

4 [g]"Ulikuwa wapi nilipoweka misingi
ya dunia?
Niambie, kama unafahamu.
5 [h]Ni nani aliyeweka alama vipimo
vyake?
Hakika wewe unajua!
Ni nani aliyenyoosha kamba ya
kupimia juu yake?
6 [i]Je, misingi yake iliwekwa juu ya
nini,
au ni nani aliyeweka jiwe la
pembeni,
7 [j]wakati nyota za asubuhi zilipoimba
pamoja,
na malaika wote walipokuwa
wakipiga kelele kwa furaha?

8 [k]"Ni nani aliyeifungia bahari milango
ilipopasuka kutoka tumbo,
9 [l]nilipoyafanya mawingu kuwa vazi
lake,
na kuyafungia katika giza nene,
10 [m]nilipoamuru mipaka yake,
na kuiweka milango yake na
makomeo mahali pake,
11 [n]niliposema, 'Unaweza kufika mpaka
hapa wala si zaidi;
hapa ndipo mawimbi yako yenye
kiburi yatakapokomea'?

12 [o]"Umepata kuiamrisha asubuhi
ipambazuke,
au kuyaonyesha mapambazuko
mahali pake,
13 yapate kushika miisho ya dunia,
na kuwakung'uta waovu waliomo?
14 [p]Dunia hubadilika kama udongo wa
mfinyanzi chini ya lakiri;
sura yake hukaa kama ile ya vazi.
15 [q]Waovu huzuiliwa nuru yao,
nao mkono wao ulioinuliwa
huvunjwa.

16 [r]"Je, umepata kufika kwenye
chemchemi za bahari?
Au kutembea mahali pa ndani pa
vilindi?
17 [s]Umewahi kuonyeshwa malango ya
mauti?
Umewahi kuiona milango ya uvuli
wa mauti?

---

[a]**37:22** Za 19:5; Kut 24:17
[b]**37:23** Ay 5:9; Rum 11:33; Ay 8:3; Yer 25:5; Mao 3:33
[c]**37:24** Mik 6:8; Mt 10:28; 11:25; Efe 5:15
[d]**38:1** 1Sam 2:10; Eze 1:4; Kut 19:16-18; Ay 11:5; 40:6; Isa 21:1
[e]**38:2** Mk 10:38; 1Tim 1:7
[f]**38:3** Ay 40:7; 42:4; Mk 11:29; 1Fal 18:46
[g]**38:4** Mwa 1:1; Mit 8:29; Za 104:5
[h]**38:5** Za 102:25; Yer 31:37
[i]**38:6** Mit 8:25; Ay 26:7
[j]**38:7** Mwa 1:16; Za 19:1-4; 148:2-3; 1Fal 22:19; Kum 16:15
[k]**38:8** Za 33:7; Yer 5:22; Mwa 1:9-10
[l]**38:9** Mwa 1:2
[m]**38:10** Za 33:7; Neh 3:3; Isa 40:12; Ay 7:12
[n]**38:11** Za 65:7; 89:9; 104:6-9
[o]**38:12** Za 57:8; 74:16; Amo 5:8
[p]**38:14** Kut 28:11
[q]**38:15** Kum 28:29; Ay 15:22; Mwa 17:14; Za 10:15
[r]**38:16** Mwa 1:7; Ay 9:8
[s]**38:17** Za 9:13; Mt 16:18

18 [a]Je, wewe unafahamu ukubwa wa
dunia?
Niambie kama unajua haya yote.

19 [b]"Njia ya kufika kwenye makao ya
nuru ni ipi?
Nako maskani mwa giza ni wapi?
20 [c]Je, unaweza kuvirudisha kwenye
makao yake?
Unajua njia za kufika maskani
mwake?
21 [d]Hakika unajua, kwa kuwa ulikuwa
umeshazaliwa!
Kwani umeishi miaka mingi!

22 [e]"Je, umeshawahi kuingia katika
ghala za theluji,
au kuona ghala za mvua ya mawe,
23 [f]ambazo nimeziweka akiba kwa ajili
ya wakati wa taabu,
na kwa ajili ya wakati wa vita na
mapigano?
24 [g]Ni ipi njia iendayo mahali umeme
wa radi unapotawanyiwa,
au mahali upepo wa mashariki
unaposambaziwa juu ya
dunia?
25 [h]Ni nani aliyepasua mifereji kwa
ajili ya maji mengi ya mvua
yaendayo kasi
na njia ya umeme wa radi,
26 [i]ili kusababisha mvua kunyeshea
mahali pasipokaliwa na mtu,
jangwa lisilo na yeyote ndani
yake,
27 [j]ili kuitosheleza nchi ya ukiwa na
jangwa,
na majani yaanze kumea ndani
yake?

28 [k]Je, mvua ina baba?
Ni nani baba azaaye matone ya
umande?
29 [l]Barafu inatoka tumbo la nani?
Ni nani azaaye ukungu kutoka
mbinguni,
30 [m]wakati maji yawapo magumu kama
jiwe,
wakati uso wa vilindi vya maji
unapoganda?

31 [n]"Je, waweza kuufunga mnyororo wa
Kilimia?
Waweza kulegeza kamba za
Orioni?
32 [o]Waweza kuyaongoza makundi ya
nyota kwa majira yake,
au kuongoza Dubu na watoto
wake?
33 [p]Je, unajua sheria zinazotawala
mbingu?
Waweza kuweka utawala wa
Mungu duniani?

34 [q]"Waweza kuiinua sauti yako mpaka
mawinguni,
na kujifunika mwenyewe na
gharika ya maji?
35 [r]Je, wewe hutuma umeme wa radi
kwenye njia zake?
Je, hutoa taarifa kwako
kukuambia, 'Sisi tuko hapa'?
36 [s]Ni nani aliyeujalia moyo hekima
au kuzipa akili ufahamu?
37 [t]Nani mwenye hekima ya
kuyahesabu mawingu?
Ni nani awezaye kuinamisha
magudulia ya mbinguni

---

[a]**38:18** Ay 28:24; Isa 40:12; Ay 38:4
[b]**38:19** Mwa 1:4; Ay 28:3; Za 139:11-12
[c]**38:20** Ay 24:13
[d]**38:21** Ay 15:7
[e]**38:22** Ay 37:6; Kum 28:12; Za 105:32; 147:17
[f]**38:23** Za 27:5; Isa 28:17; Eze 13:13; Ufu 16:21; Kut 9:18; Za 9:13
[g]**38:24** Ay 28:24; 27:21; Yer 10:13; 51:16
[h]**38:25** Ay 28:26
[i]**38:26** Ay 36:27; Za 84:6; 107:35; Isa 41:18
[j]**38:27** Ay 28:26; 37:13; Za 104:14
[k]**38:28** 2Sam 1:21; Yer 14:22
[l]**38:29** Za 147:16-17
[m]**38:30** Ay 37:10
[n]**38:31** Ay 9:9; Amo 5:8
[o]**38:32** 2Fal 23:5; Isa 13:10; 40:26; 45:12; Yer 19:13; Mwa 1:16
[p]**38:33** Za 148:6; Yer 31:38
[q]**38:34** Ay 5:10; 22:11
[r]**38:35** Ay 36:32
[s]**38:36** Ay 34:32; Yak 1:5; Za 51:6; Mhu 2:26
[t]**38:37** Yos 3:16; Ay 22:11

[38] [a]wakati mavumbi yawapo magumu,
na mabonge ya udongo
kushikamana pamoja?

[39] [b]"Je, utamwindia simba jike
mawindo,
na kuwashibisha simba wenye
njaa
[40] [c]wakati wao wamejikunyata
mapangoni mwao,
au wakivizia kichakani?
[41] [d]Ni nani ampaye kunguru chakula
wakati makinda yake yanamlilia
Mungu,
yakizungukazunguka kwa ajili ya
kukosa chakula?

39 [e]"Je, wajua ni wakati gani mbuzi
wa mlimani wanapozaa?
Je, watambua ni wakati gani
kulungu jike azaapo mtoto
wake?
[2] [f]Je, waweza kuhesabu miezi hadi
wazaapo?
Je, unajua majira yao ya kuzaa?
[3] Wao hujiinamisha na kuzaa watoto
wao;
utungu wa kuzaa unakoma.
[4] Watoto wao hustawi na kuongezeka
nguvu nyikani;
huenda zao wala hawarudi tena.

[5] [g]"Ni nani aliyemwachia punda-
mwitu awe huru?
Ni nani aliyezifungua kamba zake?
[6] [h]Nimempa nchi isiyokaliwa na watu
kuwa masikani yake,
nchi ya chumvi kuwa makao yake.
[7] [i]Huzicheka ghasia za mji,
wala hasikii kelele za mwendesha
gari.
[8] [j]Huzunguka vilimani kwa ajili ya
malisho
na kutafuta kila kitu kibichi.

[9] [k]"Je, nyati atakubali kukutumikia?
Atakaa karibu na hori lako usiku?
[10] [l]Je, waweza kumfungia kwenye
matuta kwa kamba?
Je, atalima mabonde nyuma yako?
[11] [m]Je, utamtumainia kwa ajili ya
nguvu zake nyingi?
Utamwachia yeye kazi zako nzito?
[12] Utaweza kumwamini akuletee
nafaka yako nyumbani
kutoka shambani na kuikusanya
kwenye sakafu yako ya
kupuria?

[13] [n]"Mbuni hupigapiga mabawa yake
kwa furaha,
lakini hayawezi kulinganishwa
na mabawa na manyoya ya
korongo.
[14] Huyataga mayai yake juu ya ardhi,
na kuyaacha yapate joto
mchangani,
[15] [o]bila kujali kuwa mguu waweza
kuyaponda,
kwamba baadhi ya wanyama
wa porini wanaweza
kuyakanyaga.
[16] [p]Yeye huyafanyia makinda yake
ukatili kama vile si yake;
hajali kwamba taabu yake inaweza
ikawa bure,
[17] [q]kwa kuwa Mungu hakumjalia
hekima,
wala hakumpa fungu la akili
njema.

---

[a]**38:38** Law 26:19
[b]**38:39** Mwa 49:9; Za 104:21
[c]**38:40** Ay 37:8; Mwa 49:9
[d]**38:41** Mwa 8:7; Lk 12:24; Za 147:9; Mt 6:26
[e]**39:1** Kum 14:5
[f]**39:2** Mwa 31:7-9
[g]**39:5** Mwa 16:12; Ay 6:5
[h]**39:6** Za 107:34; Yer 2:24; 14:6; Hos 8:9
[i]**39:7** Ay 5:22; 3:18
[j]**39:8** Isa 32:20
[k]**39:9** Hes 23:22; Kum 33:17
[l]**39:10** Ay 41:13; Za 32:9
[m]**39:11** Ay 40:16; 41:12, 22; Za 147:10
[n]**39:13** Zek 5:9
[o]**39:15** 2Fal 14:9
[p]**39:16** Ay 39:17; Mao 4:3
[q]**39:17** Ay 21:22; 39:16

18 [a]Lakini akunjuapo mabawa yake
kukimbia,
humcheka farasi pamoja na yeye
aliyempanda.

19 [b]"Je, wewe humpa farasi nguvu
au kuivika shingo yake manyoya
marefu?
20 [c]Je, wewe humfanya farasi aruke
kama nzige,
akistaajabisha kwa tishio la mlio
wake wa majivuno?
21 [d]Huparapara bila woga, akizifurahia
nguvu zake,
husonga mbele kukabiliana na
silaha.
22 [e]Huicheka hofu, haogopi chochote,
wala haukimbii upanga.
23 [f]Podo hutoa sauti kando yake,
pamoja na mkuki unaong'aa na
fumo.
24 [g]Bila woga na kwa ghadhabu
huimeza nchi,
wala tarumbeta iliapo yeye hawezi
kusimama.
25 [h]Asikiapo sauti ya baragumu yeye
hulia, 'Aha!'
Hunusa harufu ya vita toka mbali,
sauti ya mtoa amri na ukelele wa
vita.

26 "Je, mwewe huruka kwa hekima
yako
na kuyakunjua mabawa yake
kuelekea kusini?
27 Je, tai hupaa juu kwa amri yako
na kujenga kiota chake mahali pa
juu?
28 Huishi juu ya miamba mirefu na
kukaa huko usiku;
majabali yenye ncha kali ndiyo
ngome yake.
29 Kutoka huko hutafuta chakula chake;
macho yake hukiona kutoka
mbali.
30 [i]Makinda yake hujilisha damu,
na pale palipo na machinjo, ndipo
yeye alipo."

40 [j]BWANA akamwambia Ayubu:

2 [k]"Je, mwenye
kushindana na Mwenyezi
aweza kumsahihisha?
Mwenye kumlaumu Mungu na
ajibu."

3 Ndipo Ayubu akamjibu BWANA:

4 [l]"Mimi sistahili kabisa: ninawezaje
kukujibu wewe?
Nauweka mkono wangu juu ya
kinywa changu.
5 [m]Nimesema mara moja, lakini sina
jibu;
naam, nimesema mara mbili,
lakini sitasema tena."

6 [n]Ndipo BWANA akasema na Ayubu
kutoka upepo wa kisulisuli:

7 [o]"Jikaze kama mwanaume;
nitakuuliza maswali, nawe
yakupasa unijibu.

8 [p]"Je, utabatilisha hukumu yangu?
Utanilaumu mimi ili kujihesabia
haki mwenyewe?
9 [q]Je, una mkono kama wa Mungu,
nawe waweza kutoa sauti ya
ngurumo kama yake?

[a]**39:18** Ay 5:22
[b]**39:19** Ay 39:11
[c]**39:20** Yoe 2:4-5; Ufu 9:7; Yer 8:16
[d]**39:21** Yer 8:6
[e]**39:22** Ay 5:22
[f]**39:23** Isa 5:28; Yer 5:16; Nah 3:3
[g]**39:24** Hes 10:9; Eze 7:14
[h]**39:25** Yos 6:5; Yer 8:6; Amo 2:2
[i]**39:30** Mt 24:28; Lk 17:37
[j]**40:1** Ay 5:8; 13:3; 13:3; 9:15; 9:3; 11:8; 33:13
[k]**40:2** Rum 9:20
[l]**40:4** Ay 42:6; Amu 18:19; Ay 29:9; Ezr 9:6; Zek 2:13
[m]**40:5** Ay 9:3; 9:15
[n]**40:6** Kut 14:21; Ay 38:1
[o]**40:7** Ay 38:3
[p]**40:8** Ay 15:25; Rum 3:3; Za 51:4
[q]**40:9** 2Nya 32:8; Za 98:1; Kut 20:19; Za 29:3-4

10 [a]Basi jivike mwenyewe utukufu na
fahari,
nawe uvae heshima na enzi.
11 [b]Fungulia ukali wa ghadhabu yako,
mtafute kila mwenye kiburi
umshushe,
12 [c]mwangalie kila mtu mwenye kiburi
na umnyenyekeze,
waponde waovu mahali
wasimamapo.
13 [d]Wazike wote mavumbini pamoja;
wafunge nyuso zao kaburini.
14 [e]Ndipo mimi mwenyewe
nitakukubalia
kuwa mkono wako mwenyewe wa
kuume unaweza kukuokoa.

15 [f]"Mwangalie mnyama aitwaye
Behemothi,[g]
niliyemuumba kama
nilivyokuumba wewe,
anayekula majani kama ng'ombe.
16 [h]Tazama basi nguvu alizo nazo
kwenye viuno vyake,
uwezo alio nao kwenye misuli ya
tumbo lake!
17 [i]Mkia wake hutikisika kama
mwerezi;
mishipa ya mapaja yake imesukwa
pamoja.
18 [j]Mifupa yake ni bomba za shaba,
maungo yake ni kama fito za
chuma.
19 [k]Yeye ni wa kwanza miongoni mwa
kazi za Mungu,
lakini Muumba wake anaweza
kumsogelea kwa upanga
wake.
20 [l]Vilima humletea yeye mazao yake,
nao wanyama wote wa porini
hucheza karibu naye.
21 [m]Hulala chini ya mimea ya
yungiyungi,
katika maficho ya matete kwenye
matope.
22 [n]Hiyo mimea ya yungiyungi
humficha kwenye vivuli
vyake;
miti mirefu karibu na kijito
humzunguka.
23 Wakati mto ufurikapo, yeye hapati
mshtuko wa hofu;
yeye yu salama, hata kama
Yordani ingefurika hadi
kwenye kinywa chake.
24 [o]Je, mtu yeyote anaweza kumkamata
yeye akiwa macho,
au kumnasa kwa mtego na
kutoboa pua yake?

41 [p]"Je, waweza kumvua Lewiathani[q]
kwa ndoano ya samaki,
au kufunga ulimi wake kwa
kamba?
2 [r]Waweza kupitisha kamba puani
mwake,
au kutoboa taya lake kwa kulabu?
3 [s]Je, ataendelea kukuomba
umhurumie?
Atasema nawe maneno ya upole?
4 [t]Je, atafanya agano nawe ili umtwae
awe mtumishi wako maisha yake
yote?

---

[a]**40:10** Za 29:1-2; 45:3; 93:1; 96:6; 104:1; 145:5
[b]**40:11** Nah 1:6; Sef 1:18; Za 18:27; Isa 32:19
[c]**40:12** Za 52:5; 1Pet 5:5; Dan 5:20; Mal 4:3; Lk 18:14
[d]**40:13** Hes 16:31-34; Ay 4:9
[e]**40:14** Kut 15:6; Isa 63:5
[f]**40:15** Ay 9:9; Isa 11:7; 65:25
[g]15 Huyu alikuwa mnyama wa nyakati za zamani ambaye hajulikani hasa ni gani.
[h]**40:16** Ay 39:11; 41:9
[i]**40:17** Ay 41:15
[j]**40:18** Ay 41:12; Isa 11:4; 49:2
[k]**40:19** Za 40:5; Isa 27:1
[l]**40:20** Za 104:14, 26
[m]**40:21** Mwa 41:2; Za 68:30; Isa 35:7; Ay 8:11
[n]**40:22** Za 1:3; Isa 44:4
[o]**40:24** 2Fal 19:28; Isa 37:29
[p]**41:1** Za 104:26; Isa 27:1
[q]1 Lewiathani ni mnyama mkubwa wa baharini mwenye magamba anayefanana na joka kubwa, mwenye umbo la kutisha, asiyeweza kuvuliwa.
[r]**41:2** Isa 37:29; Eze 19:4; Isa 30:28
[s]**41:3** 1Fal 20:31
[t]**41:4** Kut 21:6

5 Je, utamfuga na kumfanya rafiki
kama ndege,
au kumfunga kamba kwa ajili ya
wasichana wako?
6 Je, wafanyabiashara watabadilishana
bidhaa kwa ajili yake?
Watamgawanya miongoni mwa
wafanyao biashara?
7 [a]Je, waweza kuijaza ngozi yake kwa
vyuma vyenye ncha kali,
au kichwa chake kwa mkuki wa
kuvulia samaki?
8 [b]Kama ukiweka mkono wako juu
yake,
utavikumbuka hivyo vita na
kamwe hutarudia tena!
9 [c]Tumaini lolote la kumtiisha ni
kujidanganya;
kule kumwona tu kunamwangusha
mtu chini.
10 [d]Hakuna yeyote aliye mkali
athubutuye kumchokoza.
Ni nani basi awezaye kusimama
dhidi yangu?
11 [e]Ni nani mwenye madai dhidi yangu
ili nipate kumlipa?
Kila kitu kilicho chini ya mbingu
ni mali yangu.

12 [f]"Sitashindwa kunena juu ya maungo
yake,
nguvu zake na umbo lake zuri.
13 [g]Ni nani awezaye kumvua gamba
lake la nje?
Ni nani awezaye kumsogelea na
lijamu?
14 [h]Nani athubutuye kuufungua mlango
wa kinywa chake,
kilichozungukwa na meno yake ya
kutisha pande zote?
15 [i]Mgongo wake una safu za ngao
zilizoshikamanishwa imara
pamoja;
16 kila moja iko karibu sana na
mwenzake,
wala hakuna hewa iwezayo kupita
kati yake.
17 Zimeunganishwa imara kila moja na
nyingine;
zimeng'ang'aniana pamoja wala
haziwezi kutenganishwa.
18 [j]Akipiga chafya mwanga
humetameta;
macho yake ni kama mionzi ya
mapambazuko.
19 [k]Mienge iwakayo humiminika kutoka
kinywani mwake;
cheche za moto huruka nje.
20 [l]Moshi hufuka kutoka puani mwake,
kama kutoka kwenye chungu
kinachotokota kwa moto wa
matete.
21 [m]Pumzi yake huwasha makaa ya
mawe,
nayo miali ya moto huruka kutoka
kinywani mwake.
22 [n]Nguvu hukaa katika shingo yake;
utisho hutangulia mbele yake.
23 Mikunjo ya nyama yake
imeshikamana imara pamoja;
iko imara na haiwezi kuondolewa.
24 [o]Kifua chake ni kigumu kama
mwamba,
kigumu kama jiwe la chini la
kusagia.
25 [p]Ainukapo, mashujaa wanaogopa;
hurudi nyuma mbele yake
anapokwenda kwa kishindo.
26 [q]Upanga unaomfikia haumdhuru,
wala mkuki au mshale wala fumo.

---

[a]**41:7** Ay 40:24
[b]**41:8** Ay 3:8
[c]**41:9** Ay 40:16
[d]**41:10** Ay 3:8; 2Nya 20:6; Ufu 6:17; 1Kor 10:22
[e]**41:11** Ay 34:33; Yos 3:11; Rum 11:35; Mdo 4:24; Mwa 14:19; Kum 10:14
[f]**41:12** Ay 40:18; 39:11
[g]**41:13** Ay 30:11; 39:10
[h]**41:14** Za 22:13
[i]**41:15** Ay 40:17
[j]**41:18** Ay 40:17
[k]**41:19** Dan 10:6
[l]**41:20** Za 18:8
[m]**41:21** Ay 4:9; Isa 11:4; 10:17; Yer 4:4
[n]**41:22** Ay 39:11
[o]**41:24** Mt 18:6
[p]**41:25** Ay 39:20; 3:8
[q]**41:26** Ay 8:18; 40:24

27 [a]Chuma hukiona kama unyasi,
na shaba kama mti uliooza.
28 [b]Mishale haimfanyi yeye akimbie;
mawe ya kombeo kwake ni kama makapi.
29 [c]Rungu kwake huwa kama kipande cha jani kavu;
hucheka sauti za kugongana kwa mkuki.
30 [d]Sehemu zake za chini kwenye tumbo
zina menomeno na mapengo kama vigae vya chungu,
zikiacha mburuzo kwenye matope
kama chombo chenye meno cha kupuria.
31 [e]Huvisukasuka vilindi kama sufuria kubwa ichemkayo,
na kukoroga bahari kama chungu cha marhamu.
32 Anapopita nyuma yake huacha mkondo unaometameta;
mtu angedhani vilindi vilikuwa na mvi.
33 [f]Hakuna chochote duniani kinacholingana naye:
yeye ni kiumbe kisicho na woga.
34 [g]Yeye huwatazama chini wale wote wenye kujivuna;
yeye ni mfalme juu ya wote wenye kiburi."

## SEHEMU YA TANO

*(Ayubu 42)*

### *Ayubu Anamjibu Bwana*

1 Ndipo Ayubu akamjibu BWANA:

2 [h]"Ninajua ya kuwa unaweza kufanya mambo yote,
wala hakuna mpango wako unaoweza kuzuilika.
3 [i]Uliuliza, 'Ni nani huyu afichaye mashauri yangu bila maarifa?'
Hakika nilisema juu ya mambo niliyokuwa siyaelewi,
mambo ya ajabu mno kwangu mimi kuyajua.

4 [j]"Ulisema, 'Sikiliza sasa, nami nitanena;
nitakuuliza swali, nawe yakupasa kunijibu.'
5 [k]Masikio yangu yalikuwa yamesikia habari zako,
lakini sasa macho yangu yamekuona.
6 [l]Kwa hiyo najidharau mwenyewe,
na kutubu katika mavumbi na majivu."

### *Mwisho: Marafiki Wa Ayubu Wanafedheheshwa*

7 [m]Baada ya BWANA kusema mambo
haya yote na Ayubu, akamwambia Elifazi
Mtemani, "Nina hasira juu yako na juu ya
rafiki zako wawili, kwa sababu hamkusema
yaliyo sawa kwa habari yangu, kama
alivyosema mtumishi wangu Ayubu. 8 [n]Basi
sasa chukueni mafahali saba na kondoo
dume saba mkamwendee mtumishi wangu
Ayubu nanyi mkatoe sadaka za kuteketezwa
kwa ajili yenu wenyewe. Mtumishi wangu
Ayubu ataomba kwa ajili yenu, nami
nitayakubali maombi yake ili nisiwatendee
sawasawa na upumbavu wenu. Ninyi
hamkusema yaliyo sawa kwa habari yangu,
kama alivyosema mtumishi wangu Ayubu."
9 [o]Kwa hiyo Elifazi Mtemani, Bildadi
Mshuhi, na Sofari Mnaamathi wakafanya
kama BWANA alivyowaambia; naye BWANA
akayakubali maombi ya Ayubu.
10 [p]Baada ya Ayubu kuwaombea rafiki

[a]**41:27** Ay 41:29
[b]**41:28** Za 91:5
[c]**41:29** Ay 41:27; 5:22
[d]**41:30** Isa 28:27; Amo 1:3; Isa 41:15
[e]**41:31** 1Sam 2:14; Eze 32:2
[f]**41:33** Ay 40:19
[g]**41:34** Ay 28:8
[h]**42:2** Mwa 18:14; Yer 32:17; Mt 19:26; 2Nya 20:6; Efe 1:11
[i]**42:3** Ay 34:35; 38:2; Za 40:5
[j]**42:4** Ay 38:3; 40:7
[k]**42:5** Ay 26:14; Rum 10:17; Amu 13:22; Mt 5:8
[l]**42:6** Eze 6:9; Rum 12:3; Kut 10:3; Ezr 9:6
[m]**42:7** Yos 1:7; Ay 32:3, 8; 9:15
[n]**42:8** Hes 23:29; Eze 45:23; Mwa 20:17; Yak 5:15-17; Ay 22:30
[o]**42:9** Ay 2:11; Mwa 19:21; 20:17; Eze 14:14
[p]**42:10** Kum 30:3; Za 14:7; 126:5-6; Yak 5:11

zake, Bwana akamwondoa kwenye uteka,
akamfanikisha tena naye akampa mara mbili
ya vile alivyokuwa navyo hapo mwanzoni.
11 [a]Ndipo ndugu zake wote waume kwa
wake na kila mtu aliyemfahamu mwanzoni,
wakaja wakala pamoja naye katika nyumba
yake. Wakamfariji na kumtuliza moyo juu
ya taabu yote Bwana aliyoileta juu yake,
nao kila mmoja akampa kipande cha fedha
na pete ya dhahabu.
12 [b]Bwana akaibariki sehemu ya mwisho
ya maisha ya Ayubu kuliko ile ya kwanza.
Alikuwa na kondoo elfu kumi na nne,
ngamia elfu sita, jozi za mafahali elfu moja,
na punda wa kike elfu moja. 13 Tena alikuwa
na wana saba na binti watatu. 14 Binti wa
kwanza aliitwa Yemima, wa pili Kesia na wa
tatu Keren-Hapuki. 15 Hapakuwepo mahali
popote katika nchi ile yote palipopatikana
wanawake wazuri kama binti za Ayubu;
naye baba yao akawapa urithi pamoja na
ndugu zao.
16 Baada ya hili Ayubu akaishi miaka 140;
akawaona wanawe na wana wa wanawe
hata kizazi cha nne. 17 [c]Hivyo Ayubu akafa,
akiwa mzee aliyekuwa ameshiba siku.

---

[a]**42:11** Ay 19:13
[b]**42:12** Yak 5:11
[c]**42:17** Mwa 15:15; 25:8

# ZABURI

KITABU CHA KWANZA

*(Zaburi 1–41)*

**Zaburi 1**

*Furaha Ya Kweli*

1 [a]Heri mtu yule ambaye
haendi katika shauri la watu waovu,
wala hasimami katika njia ya wenye dhambi,
au kuketi katika baraza la wenye mizaha.
2 [b]Bali huifurahia sheria ya BWANA,
naye huitafakari hiyo sheria usiku na mchana.
3 [c]Mtu huyo ni kama mti uliopandwa
kando ya vijito vya maji,
ambao huzaa matunda kwa majira yake
na majani yake hayanyauki.
Lolote afanyalo hufanikiwa.

*Huzuni Ya Waovu*

4 [d]Sivyo walivyo waovu!
Wao ni kama makapi
yapeperushwayo na upepo.
5 [e]Kwa hiyo waovu hawatastahimili hukumu,
wala wenye dhambi katika kusanyiko la wenye haki.

6 Kwa maana BWANA huziangalia njia za mwenye haki,
bali njia ya waovu itaangamia.

**Zaburi 2**

*Mfalme Aliyechaguliwa Na Mungu*

1 [f]Kwa nini mataifa wanashauriana kufanya mabaya,
na kabila za watu kula njama bure?
2 [gh]Wafalme wa dunia wanajipanga
na watawala wanajikusanya pamoja
dhidi ya BWANA
na dhidi ya Mpakwa Mafuta wake.
3 [i]Wanasema, "Tuvunje minyororo yao
na kuvitupilia mbali vifungo vyao."

4 [j]Yeye atawalaye mbinguni hucheka,
Bwana huwadharau.
5 [k]Kisha huwakemea katika hasira yake
na kuwaogopesha katika ghadhabu yake, akisema,
6 [l]"Nimemtawaza Mfalme wangu
juu ya Sayuni, mlima wangu mtakatifu."

*Ushindi Wa Mfalme*

7 [m]Nitatangaza amri ya BWANA:
Yeye aliniambia, "Wewe ni Mwanangu,
leo mimi nimekuzaa.

---

[a]**1:1** Kum 33:29; Za 40:4; 26:9; 37:38; 51:13; 104:35; 26:4; 10:2-11; 128:4; 89:15; 81:12; Mwa 49:6; Isa 28:14; Hos 7:5; Ay 21:16; 11:3; 31:5; Mit 1:22; 4:14
[b]**1:2** Za 19:7; 119:1, 16, 35; 112:1; Rum 7:22; Eze 11:20; 18:17; Mwa 24:63
[c]**1:3** Za 46:4; 65:9; 52:8; 92:12, 14; 128:2, 3; Yer 11:16; Zek 4:3; Hes 24:6; Ay 14:9; Eze 17:5; 47:12; Isa 1:30; 64:6; Mwa 39:3
[d]**1:4** Ay 13:25; Isa 40:24; Yer 13:24
[e]**1:5** Za 5:5; 26:12; 35:28; 82:1; 89:5; 107:32; 111:1; 149:1; Ay 19:29; 1:6; Za 37:18; 121:5; 145:20; 9:6; Nah 1:7; Law 26:38; Yn 1:41
[f]**2:1** Za 21:11; 83:5; Mit 24:2
[g]**2:2** Za 45:7; 48:4; 1Sam 9:16; Yn 1:41; Mdo 4:25-26
[h]**2:2** Mao 3:55; Za 22:2; 55:17; 142:5; 42:7
[i]**2:3** Ay 36:8; Lk 19:14; 2Sam 3:34
[j]**2:4** Za 11:4; Isa 37:16; 40:22; 66:1; Za 37:13; Mit 1:26
[k]**2:5** Za 6:1; 27:9; 38:1; 21:9; 79:6; 90:7; 110:5
[l]**2:6** Za 10:16; 24:10; 9:11; 48:2, 11; 78:6; 110:2; 133:3; 2Fal 19:31; Kut 15:17
[m]**2:7** Mt 3:17; 8:29; 2Sam 7:14; Ebr 1:5; 5:5; Mdo 13:33

8 [a]Niombe, nami nitayafanya mataifa
kuwa urithi wako,
miisho ya dunia kuwa milki yako.
9 [b]Utawatawala kwa fimbo ya chuma
na kuwavunjavunja kama chombo
cha mfinyanzi."

10 [c]Kwa hiyo, ninyi wafalme, kuweni
na hekima;
mwonyeke, enyi watawala wa
dunia.
11 [d]Mtumikieni BWANA kwa hofu
na mshangilie kwa kutetemeka.
12 [e]Mbusu Mwana, asije akakasirika
nawe ukaangamizwa katika njia
yako,
kwa maana hasira yake inaweza
kuwaka ghafula.
Heri wote wanaomkimbilia.

## Zaburi 3

*Sala Ya Asubuhi Ya Kuomba Msaada*

*Zaburi ya Daudi. Alipomkimbia mwanawe Absalomu.*

1 [f]Ee BWANA, tazama adui zangu
walivyo wengi!
Ni wengi kiasi gani wanaoinuka
dhidi yangu!
2 [g]Wengi wanasema juu yangu,
"Mungu hatamwokoa."

3 [h]Lakini wewe, Ee BWANA, ni ngao
pande zote;
umeniwekea utukufu na kuinua
kichwa changu.
4 [i]Ninamlilia BWANA kwa sauti kuu,
naye ananijibu kutoka mlima
wake mtakatifu.

5 [j]Ninajilaza na kupata usingizi;
naamka tena, kwa maana BWANA
hunitegemeza.
6 [k]Sitaogopa makumi elfu ya adui,
wanaojipanga dhidi yangu kila
upande.

7 [l]Ee BWANA, amka!
Niokoe, Ee Mungu wangu!
Wapige adui zangu wote kwenye
taya,
vunja meno ya waovu.

8 [m]Kwa maana wokovu watoka kwa
BWANA.
Baraka yako na iwe juu ya watu
wako.

## Zaburi 4

*Sala Ya Jioni Ya Kuomba Msaada*

*Kwa mwimbishaji. Kwa ala za nyuzi za muziki. Zaburi ya Daudi.*

1 [n]Nijibu nikuitapo,
Ee Mungu wangu mwenye haki!
Nipumzishe katika shida zangu;
nirehemu, usikie ombi langu.

2 [o]Enyi watu, mtabadilisha utukufu
wangu
kuwa aibu mpaka lini?
Mtapenda udanganyifu
na kufuata miungu ya uongo
mpaka lini?

---

[a]**2:8** Ay 22:26; Za 22:27; 67:7; Dan 7:13, 14; Mt 21:38
[b]**2:9** Mwa 49:10; Ufu 2:27; 12:5; 19:15; Mt 21:44; Kut 15:6; Isa 30:14; Yer 19:10
[c]**2:10** Za 141:6; Amu 2:3; Mit 8:15; 27:11
[d]**2:11** 1Nya 16:30; Za 9:2; 35:9; Isa 61:10
[e]**2:12** Kum 9:8; Za 5:11; 34:8; 64:10; Yer 17:7; Ufu 6:16; Yn 5:22, 23
[f]**3:1** 1Sam 15:12
[g]**3:2** Za 22:8; 22:7, 8; 71:11
[h]**3:3** Mwa 15:1; Za 27:6; 2Fal 25:27
[i]**3:4** Ay 30:20; Za 2:6; 27:6
[j]**3:5** Law 26:6; Mdo 12:6; Za 4:8; 17:15; 139:18; Mit 3:24
[k]**3:6** Za 23:4; 27:3; 118:11; Ay 11:15
[l]**3:7** 2Nya 6:41; Mt 6:13; Za 6:4; 7:1; 59:1; 57:4; 109:21; 119:153; Isa 25:9; 33:22; 35:4; 36:15; 37:20; Yer 42:11; Mao 3:16; Ay 16:10; 29:17; Mit 30:14
[m]**3:8** Za 27:1; 37:39; 62:1; Hes 6:23; Isa 43:3, 11; 44:6, 8; 45:21; Hos 13:4; Yon 2:9; Mit 21:31; Za 29:11; 129:8
[n]**4:1** Za 13:3; 27:7; 69:16; 30:10; 54:2; 84:8; 88:2; 6:7; 102:2; Mwa 32:7; Amu 2:15
[o]**4:2** Kut 16:7; Amo 2:4; 2Fal 19:26; Ay 8:22; Yer 13:25; 16:19; Za 12:1; 40:4; 1Sam 4:21

3 [a]Fahamuni hakika kwamba BWANA
amewatenga
wale wamchao kwa ajili yake;
BWANA atanisikia nimwitapo.

4 [b][c]Katika hasira yako, usitende
dhambi.
Mkiwa vitandani mwenu, mtulie
kimya
mkiichunguza mioyo yenu.
5 [d][e]Toeni dhabihu zilizo haki;
mtegemeeni BWANA.

6 [f]Wengi wanauliza, "Ni nani awezaye
kutuonyesha jema lolote?"
Ee BWANA, tuangazie nuru ya uso
wako.
7 [g]Wewe umejaza moyo wangu kwa
furaha kubwa
kuliko watu waliopata nafaka na
divai kwa wingi.
8 [h][i]Nitajilaza chini na kulala kwa
amani,
kwa kuwa wewe peke yako, Ee
BWANA,
waniwezesha kukaa kwa salama.

## Zaburi 5

*Sala Kwa Ajili Ya Ulinzi Wakati Wa Hatari*

*Kwa mwimbishaji. Kwa filimbi. Zaburi ya Daudi.*

1 [j]Ee BWANA, tegea sikio maneno
yangu,
uangalie kupiga kite kwangu.
2 [k]Sikiliza kilio changu ili unisaidie,
Mfalme wangu na Mungu wangu,
kwa maana kwako ninaomba.
3 [l]Asubuhi, unasikia sauti yangu, Ee
BWANA;
asubuhi naleta haja zangu mbele
zako,
na kusubiri kwa matumaini.

4 [m]Wewe si Mungu unayefurahia uovu,
kwako mtu mwovu hataishi.
5 [n]Wenye kiburi hawawezi kusimama
mbele yako,
unawachukia wote watendao
mabaya.
6 [o]Unawaangamiza wasemao uongo.
BWANA huwachukia
wamwagao damu na
wadanganyifu.

7 [p]Lakini mimi, kwa rehema zako kuu,
nitakuja katika nyumba yako,
kwa unyenyekevu, nitasujudu
kuelekea Hekalu lako takatifu.
8 [q]Niongoze katika haki yako, Ee
BWANA,
kwa sababu ya adui zangu,
nyoosha njia yako mbele yangu.

9 [r][s]Hakuna neno kinywani mwao
linaloweza kuaminika,
mioyo yao imejaa maangamizi.
Koo lao ni kaburi lililo wazi,
kwa ndimi zao, wao hunena
udanganyifu.

---

[a]**4:3** Za 6:8; 12:1; 30:4; 31:23; 79:2; Mik 7:2, 7; Kut 33:16; 1Tim 4:7; 2Pet 3:11
[b]**4:4** Efe 4:26; Za 63:6; Dan 2:28; Mit 3:7
[c]**4:4** Za 11:1; 25:20; 31:2; 32:11
[d]**4:5** Za 31:6; 37:3; 115:9; Mit 3:5; 28:26; Kum 33:19; Yn 14:1; Isa 26:4
[e]**4:5** Hes 14:18; Isa 65:6-7; Yer 32:17
[f]**4:6** Hes 6:25; Za 80:3
[g]**4:7** Mdo 14:17; Isa 9:3; 35:10; 65:14, 18; Mwa 27:28; Kum 28:51
[h]**4:8** Law 26:6; Hes 6:26; Yer 32:37; Ay 11:18; Flp 4:7; Kum 12:10; 33:28; Yn 14:27
[i]**4:8** Law 11:44
[j]**5:1** 1Fal 8:29; Za 17:1; 38:9; 40:1; 116:2; Dan 9:18; Isa 35:10; 51:11
[k]**5:2** Ay 19:7; 24:12; 36:5; Za 44:4; 68:24; 84:3
[l]**5:3** Isa 28:19; 50:4; Yer 21:12; Sef 3:5; Eze 46:13; Hab 2:1; Rum 8:19; Za 30:5; 62:1; 119:81; 130:5
[m]**5:4** Za 1:5; 11:5; 104:35; Mit 2:22; Mal 2:17
[n]**5:5** 2Fal 19:32; Za 1:5; 45:10; 1:3; 119:104; 73:3; 75:4; 14:1; Isa 33:19; 37:33; Mit 8:13; Hab 1:13
[o]**5:6** Mit 19:22; Yn 8:44; Mdo 5:3; Ufu 21:8
[p]**5:7** Kum 13:4; Yer 44:10; Dan 6:26; 2Sam 12:16; Za 138:2; 1Fal 8:48
[q]**5:8** Za 23:3; 31:1; 71:2; 85:13; 89:16; Mit 8:20; 1Fal 8:36; Yn 1:23
[r]**5:9** Yer 5:16; Lk 11:44; Za 12:2; 28:3; 36:3; Yer 9:8; Rum 3:13
[s]**5:9** Isa 13:8; Yer 46:5

10 [a]Uwatangaze kuwa wenye hatia, Ee
Mungu!
Hila zao ziwe anguko lao
wenyewe.
Wafukuzie mbali kwa sababu ya
dhambi zao nyingi,
kwa kuwa wamekuasi wewe.

11 [b]Lakini wote wakimbiliao kwako na
wafurahi,
waimbe kwa shangwe daima.
Ueneze ulinzi wako juu yao,
ili wale wapendao jina lako
wapate kukushangilia.
12 [c]Kwa hakika, Ee BWANA,
unawabariki wenye haki,
unawazunguka kwa wema wako
kama ngao.

## Zaburi 6

*Sala Kwa Ajili Ya Msaada Wakati Wa Taabu*

*Kwa mwimbishaji. Kwa ala za nyuzi za muziki. Mtindo wa sheminithi.[d] Zaburi ya Daudi.*

1 [e]Ee BWANA, usinikemee katika
hasira yako,
wala usiniadhibu katika ghadhabu
yako.
2 [f]Unirehemu BWANA,
kwa maana nimedhoofika;
Ee BWANA, uniponye,
kwa maana mifupa yangu
ina maumivu makali.
3 [g]Nafsi yangu ina uchungu mwingi.
Mpaka lini, Ee BWANA, mpaka
lini?

4 [h]Geuka Ee BWANA, unikomboe,
uniokoe kwa sababu ya fadhili
zako.
5 [i]Hakuna mtu anayekukumbuka
akiwa amekufa.
Ni nani awezaye kukusifu
akiwa kuzimu?

6 [j]Nimechakaa kwa kulia kwa huzuni;
usiku kucha nafurikisha
kitanda changu kwa machozi;
nimelowesha viti vyangu vya fahari
kwa machozi.
7 [k]Macho yangu yamedhoofika kwa
kuhuzunika,
yamedhoofika kwa sababu ya adui
zangu wote.

8 [l]Kaeni mbali nami, ninyi nyote
mtendao mabaya,
kwa maana BWANA amesikia kulia
kwangu.
9 [m]BWANA amesikia kilio changu kwa
huruma,
BWANA amekubali sala yangu.
10 [n]Adui zangu wote wataaibika na
kufadhaika,
watarudi nyuma kwa aibu ya
ghafula.

---

[a]**5:10** Mao 1:5; 3:42; Za 78:40; 106:7; 107:11
[b]**5:11** 1Kor 2:9; Za 33:1; 81:1; 90:14; 92:4; 95:1; 145:7; 69:36; 119:132; Ay 22:19
[c]**5:12** Za 112:2; 32:7; Mwa 15:1
[d]*Sheminithi* ni mtajo mmojawapo katika lugha ya uimbaji.
[e]**6:1** Za 2:5
[f]**6:2** Za 4:1; 26:11; 61:2; 77:3; 142:3; Yer 3:12; 8:18; 12:15; 31:20; Hos 6:1; Isa 40:31; Za 32:3; 38:3; 42:10; 102:3
[g]**6:3** Ay 7:11; Za 4:2; 31:7; 38:8; 55:4; 89:46; Yn 12:27; Isa 6:11; Rum 9:2; 2Kor 2:4; Hab 1:12; 1Sam 1:14; 1Fal 18:21; Yer 4:14; Mt 26:38; Mit 18:14
[h]**6:4** Za 25:16; 69:16; 71:2; 86:16; 88:2; 102:2; 119:132; 13:5; 31:2, 16; 77:8; 85:7; 119:41; Isa 54:8, 10
[i]**6:5** Za 30:9; 88:10-12; 115:17; Isa 38:18; Mhu 9:10
[j]**6:6** Ay 3:24; 16:16; 7:3; Lk 7:38; Za 77:3; 102:5; 12:5; Mdo 20:19; Mao 1:8, 11, 21, 22; Amu 8:5
[k]**6:7** Ay 16:8; Za 31:9; 69:3; 119:82; Isa 38:14
[l]**6:8** Za 119:115; 5:5; 139:19; Mt 7:23
[m]**6:9** Za 31:22; 116:1; 3:4; 40:1, 2; 28:6
[n]**6:10** 2Fal 19:26; Za 40:14

## Zaburi 7

*Sala Ya Mtu Anayedhulumiwa*

*Ombolezo la Daudi kwa Bwana kwa sababu ya Kushi, Mbenyamini.*

1 [a]Ee Bwana, Mungu wangu,
ninakukimbilia wewe,
uniokoe na kunikomboa na wote
wanaonifuatia,
2 [b]la sivyo watanirarua kama simba
na kunichana vipande vipande,
asiwepo wa kuniokoa.

3 [a]Ee Bwana, Mungu wangu, kama
nimetenda haya
na kuna hatia mikononi mwangu,
4 [d]au ikiwa nimemtenda uovu aliye na
amani nami,
au nimemnyang'anya adui yangu
pasipo sababu,
5 [e]basi adui anifuatie na kunipata,
auponde uhai wangu ardhini
na kunilaza mavumbini.

6 [f]Amka kwa hasira yako, Ee Bwana,
inuka dhidi ya ghadhabu ya adui
zangu.
Amka, Mungu wangu, uamue haki.
7 [g]Kusanyiko la watu na likuzunguke.
Watawale kutoka juu.
8 [h]Bwana na awahukumu kabila za
watu.
Nihukumu Ee Bwana,
kwa kadiri ya haki yangu,
kwa kadiri ya uadilifu wangu,
Ewe Uliye Juu Sana.
9 [i]Ee Mungu mwenye haki,
uchunguzaye mawazo na mioyo,
komesha ghasia za waovu
na ufanye wenye haki waishi kwa
amani.

10 [j]Ngao langu ni Mungu Aliye Juu
Sana,
awaokoaye wanyofu wa moyo.
11 [k]Mungu ni mwamuzi mwenye haki,
Mungu aghadhibikaye kila siku.
12 [l]Kama hakutuhurumia,
atanoa upanga wake,
ataupinda na kuufunga uzi upinde
wake.
13 [m]Ameandaa silaha zake kali,
ameweka tayari mishale yake ya
moto.

14 [n]Yeye aliye na mimba ya uovu
na achukuaye mimba ya ghasia
huzaa uongo.
15 [o]Yeye achimbaye shimo na kulifukua
hutumbukia katika shimo
alilochimba mwenyewe.
16 [p]Ghasia azianzishazo humrudia
mwenyewe,
ukatili wake humrudia kichwani.

17 [q]Nitamshukuru Bwana kwa ajili ya
haki yake,
na nitaliimbia sifa jina la Bwana
Aliye Juu Sana.

---

[a]**7:1** Za 2:12; 11:1; 31:1; 3:7; 31:15; 119:86, 157, 161
[b]**7:2** Mwa 49:9; Ufu 4:7; Za 3:2; 71:11; 1Pet 5:8
[a]**7:3** Za 35:7, 19; Mit 24:28; 1Sam 24:7
[d]**7:4** Za 35:7, 19; Mit 24:28; 1Sam 24:7
[e]**7:5** Kut 15:9; Ay 7:21; 2Sam 22:43; 2Fal 9:33; Isa 10:6; Mao 3:16
[f]**7:6** 2Nya 6:41; Za 138:7; 35:23; 44:23; 94:2
[g]**7:7** Za 68:18
[h]**7:8** 1Nya 16:33; Mk 5:7; 1Sam 26:23; Za 18:20; Mwa 3:5; 20:5; Hes 24:16
[i]**7:9** Yer 11:20; Ufu 2:23; Za 26:2; 37:23; 40:2; 1Sam 16:7; 1Nya 28:9
[j]**7:10** Za 3:3; Ay 33:3
[k]**7:11** Mwa 18:25; Za 9:8; 67:4; 75:2; 96:13; 98:9; Isa 11:4; Yer 11:20
[l]**7:12** Eze 3:19; 33:9; Kum 32:4; Za 21:12; 2Sam 22:35; Isa 5:28; 13:18
[m]**7:13** Za 11:2; 18:14; 64:3
[n]**7:14** Isa 59:4; Yak 1:15
[o]**7:15** Za 35:7, 8; 40:2; 94:13; Mit 26:27; Ay 4:8; Es 7:10; Mit 5:22
[p]**7:16** 1Fal 2:23
[q]**7:17** 2Nya 31:2; Za 5:8; Rum 15:11; Mwa 14:18; Ebr 2:12

## Zaburi 8

*Utukufu Wa Mungu Na Heshima Ya Mwanadamu*

*Kwa mwimbishaji. Mtindo wa gitithi. Zaburi ya Daudi.*

1 [a]Ee BWANA, Bwana wetu,
tazama jinsi lilivyo tukufu jina
lako duniani mwote!

Umeuweka utukufu wako
juu ya mbingu.
2 [b]Midomoni mwa watoto wachanga
na wanyonyao
umeamuru sifa,
kwa sababu ya watesi wako,
kumnyamazisha adui na mlipiza
kisasi.

3 [c]Nikiziangalia mbingu zako,
kazi ya vidole vyako,
mwezi na nyota,
ulizoziratibisha,
4 [d]mwanadamu ni kitu gani hata
unamfikiria,
binadamu ni nani hata unamjali?
5 [e]Umemfanya chini kidogo kuliko
viumbe wa mbinguni,
ukamvika taji ya utukufu na
heshima.

6 [f]Umemfanya mtawala juu ya kazi za
mikono yako;
umeweka vitu vyote chini ya
miguu yake.
7 [g]Mifugo na makundi yote pia,
naam, na wanyama wa kondeni,
8 [h]ndege wa angani na samaki wa
baharini,
naam, kila kiogeleacho katika njia
za bahari.

9 [i]Ee BWANA, Bwana wetu,
tazama jinsi lilivyo tukufu jina
lako duniani mwote!

## Zaburi 9[j]

*Shukrani Kwa Mungu Kwa Ajili Ya Haki Yake*

*Kwa mwimbishaji. Mtindo wa muth-labeni.[k] Zaburi ya Daudi.*

1 [l]Ee BWANA, nitakutukuza kwa moyo
wangu wote,
nitayasimulia matendo yako yote
ya ajabu.
2 [m]Nitafurahi na kushangilia ndani
yako.
Nitaliimbia sifa jina lako, Ewe
Uliye Juu Sana.

3 Adui zangu wamerudi nyuma,
wamejikwaa na kuangamia mbele
zako.
4 [n]Kwa maana umetetea haki yangu na
msimamo wangu;
umeketi kwenye kiti chako cha
enzi,
ukihukumu kwa haki.
5 [o]Umekemea mataifa na
kuwaangamiza waovu;
umeyafuta majina yao milele na
milele.

---

[a]**8:1** 1Nya 16:10; Lk 2:9; Hab 3:3; Kut 15:11; Za 57:5; 108:5; 113:4; 148:13
[b]**8:2** Mt 11:25; 21:16; Za 143:12; 1Kor 1:27
[c]**8:3** Mwa 1:16; 15:5; Kum 10:14; Kut 8:19; 1Kor 15:41; 1Nya 16:26; 2Nya 2:12; Za 102:25
[d]**8:4** 1Nya 29:14; Ebr 2:6; Ay 7:17; Za 144:3
[e]**8:5** Mwa 1:26; Za 21:5; 103:4
[f]**8:6** Mwa 1:28; Ay 10:3; Za 19:1; 102:25; 145:10; Isa 26:12; 29:23; 45:11; Ebr 1:10; 2:6-8; 1Fal 5:3; 1Kor 15:25, 27; Efe 1:22; 1Kor 15:27
[g]**8:7** Mwa 13:5; 26:14; 2:19
[h]**8:8** Mwa 1:26
[i]**8:9** Ay 11:7; Za 35:10
[j]Zaburi hii ikiunganishwa na ya 10 zimetungwa kila beti likianzia na herufi ya alfabeti ya Kiebrania zikifuatana tangu Aleph (A) hadi Taw (T); zote ni 22.
[k]Muth-labeni ni mtajo mmojawapo katika lugha za muziki.
[l]**9:1** Za 86:12; 11:1; 119:2, 10; 145:5; 138:1; Kum 4:34
[m]**9:2** Ay 22:19; Isa 25:9; Za 14:7; 31:7; 70:4; 92:1; 97:8; 126:3; Mit 23:15; Yoe 2:21; Ufu 19:7; Yer 30:19; Sef 3:14; Mt 5:12; 2Nya 31:2
[n]**9:4** 1Fal 8:45; Isa 6:1; Ay 16:21; Za 7:11; 11:4; 47:8; 67:4; 98:9; 1Pet 2:23
[o]**9:5** Mwa 20:7; 37:10; 1Nya 16:21; Za 59:5; 105:14; Isa 26:14; 66:15; Ay 18:17; Kum 9:14

6 [a]Uharibifu usiokoma umempata adui,
umeing'oa miji yao;
hata kumbukumbu lao
limetoweka.

7 [b]Bwana anatawala milele,
ameweka kiti chake cha enzi apate
kuhukumu.
8 [cd]Mungu atahukumu ulimwengu kwa
haki,
atatawala mataifa kwa haki.
9 Bwana ni kimbilio la watu
wanaoonewa,
ni ngome imara wakati wa shida.
10 [e]Wote wanaolijua jina lako
watakutumaini wewe,
kwa maana wewe Bwana,
hujawaacha kamwe wakutafutao.

11 [f]Mwimbieni Bwana sifa, amefanywa
mtawala Sayuni,
tangazeni miongoni mwa mataifa,
yale aliyoyatenda.
12 [g]Kwa maana yeye alipizaye kisasi
cha damu hukumbuka,
hapuuzi kilio cha wanaoonewa.

13 [h]Ee Bwana, tazama jinsi
walivyo wengi adui zangu
wanaonitesa!
Nihurumie, uniinue kutoka
malango ya mauti,
14 [i]ili niweze kutangaza sifa zako
katika malango ya Binti Sayuni
na huko niushangilie wokovu
wako.
15 [j]Mataifa wameanguka kwenye shimo
walilolichimba,
miguu yao imenaswa kwenye
wavu walioufícha.
16 [k]Bwana anajulikana kwa haki yake,
waovu wamenaswa katika kazi za
mikono yao.

17 [l]Waovu wataishia kuzimu,
naam, mataifa yote wanaomsahau
Mungu.
18 [m]Lakini mhitaji hatasahaulika siku
zote,
wala matumaini ya walioonewa
hayatapotea.

19 [n]Ee Bwana, inuka, usimwache
binadamu ashinde.
Mataifa na yahukumiwe mbele
zako.
20 [o]Ee Bwana, wapige kwa hofu,
mataifa na yajue kuwa wao ni
watu tu.

### Zaburi 10[p]

*Sala Kwa Ajili Ya Haki*

1 [q]Kwa nini, Ee Bwana, unasimama
mbali?
Kwa nini unajificha wakati wa
shida?

---

[a]**9:6** Kum 29:28; Yer 2:3; Mhu 9:5; Isa 14:22; 26:14; Sef 2:8-10; Za 34:16; 109:15
[b]**9:7** Mik 5:2; Ufu 19:6; Ebr 1:11; Hab 1:12; Za 90:2; 1Nya 16:31
[c]**9:8** Za 7:11; 11:7; 45:6; 72:2
[d]**9:8** Kum 33:27; 2Sam 22:3; Za 10:18; 32:7; 74:21; 121:7
[e]**9:10** Mwa 28:15; Kum 4:31; Za 22:1; 37:25; 71:11; 70:4; 91:14; Isa 49:14; Yer 15:18; Ebr 13:5; Yn 17:3; 2Kor 4:6; 1Yn 2:3, 4; 2Tim 1:12
[f]**9:11** Za 7:17; 2:6; 57:9; 18:49; 44:11; 105:1; 106:27; Isa 24:13; Eze 20:23; 1Tim 3:16
[g]**9:12** 2Sam 4:11; Za 10:17; 22:24; Isa 49:13
[h]**9:13** Hes 10:9; Za 3:7; 18:3; 6:2; 41:4; 51:1; 86:3, 16; 119:132; Ay 17:16; Mt 16:18
[i]**9:14** 2Fal 19:21; Isa 1:8; 10:32; 37:22; 62:11; Yer 4:31; 6:2; Mao 1:6; Mt 21:5; Mik 1:13; Sef 3:14; Zek 2:10; Yn 12:15
[j]**9:15** Ay 4:8; Za 35:7, 8; 57:6
[k]**9:16** Kut 7:5; Mt 5:22
[l]**9:17** Hes 16:30; Mt 5:5; Za 50:22; Ay 8:13; Hos 2:13; Yer 2:32
[m]**9:18** Za 25:3; 39:7; 71:5; Mt 23:18; Yer 14:8, 12; Za 74:19; 12:5; Flp 1:20
[n]**9:19** 2Nya 14:11; Za 3:7; 110:6; Isa 2:4; Yoe 3:12
[o]**9:20** Mwa 35:5; Isa 13:8; Lk 21:26; Za 31:13; 62:9; Isa 31:3; Eze 28:2
[p]Zaburi hii ikiunganishwa na ya 9 zimetungwa kila beti likianzia na herufi ya alfabeti ya Kiebrania zikifuatana tangu Aleph (A) hadi Taw (T); zote ni 22.
[q]**10:1** Za 13:1; 22:1, 11; 35:22; 38:21; 71:12

[2] [a]Katika kiburi chake, mwovu
humtesa maskini,
waovu na wanaswe katika hila
wanazozitunga.
[3] Hujivunia tamaa za moyo wake;
humbariki mlafi na kumtukana
BWANA.
[4] [b]Katika kiburi chake, mwovu
hamtafuti Mungu,
katika mawazo yake yote
hakuna nafasi ya Mungu.
[5] [c]Njia zake daima hufanikiwa;
hujivuna na amri zako ziko mbali
naye,
huwacheka kwa dharau adui zake
wote.
[6] [d]Anajisemea mwenyewe, "Hakuna
kitakachonitikisa,
daima nitakuwa na furaha,
kamwe sitakuwa na shida."
[7] [e]Kinywa chake kimejaa laana, uongo
na vitisho;
shida na ubaya viko chini ya ulimi
wake.
[8] [f]Huvizia karibu na vijiji;
kutoka mafichoni huwanasa wasio
na hatia,
akivizia wapitaji.
[9] [g]Huvizia kama simba aliye
mawindoni;
huvizia kumkamata mnyonge,
huwakamata wanyonge na
kuwaburuza
katika wavu wake.
[10] [h]Mateka wake hupondwa, huzimia;
wanaanguka katika nguvu zake.
[11] [i]Anajisemea mwenyewe, "Mungu
amesahau,
huficha uso wake na haoni
kabisa."

[12] [j]Inuka BWANA! Inua mkono wako,
Ee Mungu.
Usiwasahau wanyonge.
[13] [k]Kwa nini mtu mwovu anamtukana
Mungu?
Kwa nini anajiambia mwenyewe,
"Hataniita nitoe hesabu?"
[14] [l]Lakini wewe, Ee Mungu, unaona
shida na huzuni,
umekubali kuyapokea mkononi
mwako.
Mhanga anajisalimisha kwako,
wewe ni msaada wa yatima.
[15] [m]Vunja mkono wa mtu mwovu na
mbaya,
mwite atoe hesabu ya maovu yake
ambayo yasingejulikana.

[16] [n]BWANA ni Mfalme milele na milele,
mataifa wataangamia watoke
nchini mwake.
[17] [o]Unasikia, Ee BWANA, shauku ya
wanaoonewa,
wewe huwatia moyo, na kusikiliza
kilio chao,
[18] [p]ukiwatetea yatima na walioonewa,
ili mwanadamu, ambaye ni
udongo, asiogopeshe tena.

## Zaburi 11

*Kumtumaini BWANA*

*Kwa mwimbishaji. Zaburi ya Daudi.*

[1] [q]Kwa BWANA ninakimbilia,
unawezaje basi kuniambia:
"Ruka kama ndege kwenye mlima
wako.

[a]**10:2** Ay 20:19; Mit 5:22; 10:3; Za 49:6; 94:4; Yer 48:30; Ay 1:5
[b]**10:4** Za 12:3-5; 36:1; 2Fal 18:35; Ay 21:15
[c]**10:5** Za 18:27; 105:5; Mit 6:17; Isa 13:11; Yer 48:29
[d]**10:6** Ufu 18:7
[e]**10:7** Mhu 4:1; Rum 3:14; Isa 30:12; Ay 20:12; Za 73:8; 119:134
[f]**10:8** Za 37:32; 59:3; 71:10; Mit 1:11; Yer 5:26; Mik 7:2; Hos 6:9
[g]**10:9** Ay 18:8
[h]**10:10** Ay 9:17
[i]**10:11** Ay 22:13; 22:14; Za 42:9; 77:9
[j]**10:12** Za 3:7; 9:12, 13; 17:7; 20:6; 106:26; Isa 26:11; Mik 5:9
[k]**10:13** Ay 31:14
[l]**10:14** Za 22:11; 37:5; Kum 33:29
[m]**10:15** Ay 31:22
[n]**10:16** Kut 15:18; Kum 8:20
[o]**10:17** Za 9:12; Kut 22:23
[p]**10:18** Kum 24:17; Za 146:9; 9:9
[q]**11:1** Za 7:1; 50:11; Mwa 14:10

2 [a]Hebu tazama, waovu wanapinda
pinde zao,
huweka mishale kwenye uzi wake,
wakiwa gizani ili kuwapiga
wale wanyofu wa moyo.
3 [b]Wakati misingi imeharibiwa,
mwenye haki anaweza kufanya
nini?”

4 [c]BWANA yuko ndani ya Hekalu lake
takatifu;
BWANA yuko kwenye kiti chake
cha enzi mbinguni.
Huwaangalia wana wa watu,
macho yake yanawajaribu.
5 [d]BWANA huwajaribu wenye haki,
lakini waovu na wanaopenda
jeuri,
nafsi yake huwachukia.
6 [e]Atawanyeshea waovu makaa ya
moto mkali
na kiberiti kinachowaka,
upepo wenye joto kali ndio fungu
lao.

7 [f]Kwa kuwa BWANA ni mwenye haki,
yeye hupenda haki.
Wanyofu watauona uso wake.

## Zaburi 12

*Kuomba Msaada*

*Kwa mwimbishaji. Mtindo wa sheminithi. Zaburi ya Daudi.*

1 [g]BWANA tusaidie, kwa kuwa wacha
Mungu wametoweka;
waaminifu wametoweka miongoni
mwa wanadamu.
2 [h]Kila mmoja humwambia jirani yake
uongo;
midomo yao ya hila huzungumza
kwa udanganyifu.

3 [i]BWANA na akatilie mbali midomo
yote ya hila
na kila ulimi uliojaa majivuno,
4 [j]ule unaosema, “Kwa ndimi zetu
tutashinda;
midomo ni mali yetu, bwana wetu
ni nani?”

5 [k]“Kwa sababu ya uonevu wa
wanyonge
na kulia kwa uchungu kwa
wahitaji,
nitainuka sasa,” asema BWANA.
“Nitawalinda kutokana na wale
wenye nia mbaya juu yao.”
6 [l]Maneno ya BWANA ni safi,
kama fedha iliyosafishwa katika
tanuru,
iliyosafishwa mara saba.

7 [m]Ee BWANA, utatuweka salama
na kutulinda na kizazi hiki milele.
8 [n]Watu waovu huenda wakiringa kila
mahali
wakati ambapo yule aliye mbaya
sana
ndiye anayeheshimiwa miongoni
mwa watu.

---

[a]**11:2** Za 7:10, 13; 10:8; 58:7; 2Sam 22:35; Ay 33:3
[b]**11:3** Za 18:15; 82:5; Isa 24:18
[c]**11:4** 1Fal 8:48; Za 18:6; 27:4; 33:18; 66:7; Yon 2:7; Mik 1:2; Hab 2:20; Ufu 4:2; Mt 5:34; 23:22; Mit 15:3; Efe 5:13; Ebr 4:13
[d]**11:5** Ay 5:17; 23:10; 28:28; Za 94:12; 5:5; 45:7; Isa 1:14; Kum 7:13
[e]**11:6** Ufu 9:17; Ay 1:19; Mwa 9:24; 41:6
[f]**11:7** 2Nya 12:6; Ezr 9:15; Za 9:8; 33:5; 99:4; 17:15; 140:13; 2Tim 4:8; Yer 9:24; Isa 28:17; 30:18; 56:1; 61:8; Ay 1:1; Lk 23:50
[g]**12:1** Isa 57:1; Mik 7:12
[h]**12:2** Za 5:6; 34:13; 141:3; 5:9; Mt 6:19; 12:17; 13:3; Isa 32:7; Rum 16:18
[i]**12:3** Mit 26:28; 28:23; Za 73:9; Ufu 13:5; Dan 7:8; Yak 3:5
[j]**12:4** Mt 18:21; Yak 3:6
[k]**12:5** Kut 3:7, 8; Mhu 4:1, 5, 8; Isa 3:15; 5:7; 30:12; 59:13; Mdo 7:34; Za 44:24; 62:10; 72:14; 73:8; 6:6; 3:7; 34:6; 35:10
[l]**12:6** 2Sam 22:31; Isa 48:10; Za 18:30; 119:140; Ay 23:10; 28:1; Zek 13:9
[m]**12:7** Za 16:1; 27:5; 37:28; Yn 17:12
[n]**12:8** Za 55:10-11

## Zaburi 13

*Sala Ya Kuomba Msaada*

*Kwa mwimbishaji. Zaburi ya Daudi.*

1 [a][b]Mpaka lini, Ee BWANA? Je,
utanisahau milele?
Utanificha uso wako mpaka lini?
2 [c]Nitapambana na mawazo yangu
mpaka lini,
na kila siku kuwa na majonzi
moyoni mwangu?
Adui zangu watanishinda mpaka
lini?

3 [d]Nitazame, unijibu, Ee BWANA
Mungu wangu.
Yatie nuru macho yangu,
ama sivyo nitalala usingizi wa
mauti.
4 [e]Adui yangu atasema,
"Nimemshinda,"
nao adui zangu watashangilia
nitakapoanguka.

5 [f]Lakini ninategemea upendo wako
usiokoma;
moyo wangu unashangilia katika
wokovu wako.
6 [g]Nitamwimbia BWANA,
kwa kuwa amekuwa mwema
kwangu.

[a]**13:1** Mao 5:20; Kum 31:17; Za 6:3; 22:1, 14; 42:9; Isa 8:17; 54:9; 59:2; Ay 13:24
[b]**13:1** Kum 26:7; 32:20
[c]**13:2** Za 42:4; 55:2; 94:3; 139:23; Isa 33:18; Dan 7:28
[d]**13:3** Za 4:1; 9:12; 31:7; 18:28; 25:18; 35:23; 59:4; 80:14; 107:41; 119:50, 53; Lk 2:32; Efe 5:14; Ufu 21:23; Isa 37:36
[e]**13:4** 1Fal 19:2; Za 25:2; 38:16; 118:13
[f]**13:5** Ay 33:26; Isa 25:9; 33:2; Za 6:4; 9:14; 2Nya 20:12
[g]**13:6** Kut 15:1; Za 7:17

## Zaburi 14

*Uovu Wa Wanadamu*

**(Zaburi 53)**

*Kwa mwimbishaji. Zaburi ya Daudi.*

1 [h]Mpumbavu anasema moyoni
mwake,
"Hakuna Mungu."
Wameharibika, matendo yao ni
maovu kabisa;
hakuna hata mmoja atendaye
mema.

2 [i]BWANA anawachungulia wanadamu
chini
kutoka mbinguni
aone kama wako wenye akili,
wowote wanaomtafuta Mungu.
3 [j]Wote wamepotoka,
wameharibika wote pamoja,
hakuna atendaye mema.
Naam, hakuna hata mmoja!

4 [k]Je, watendao mabaya kamwe
hawatajifunza:
wale ambao huwala watu wangu
kama watu walavyo mkate,
hao ambao hawamwiti BWANA?
5 Wako hapo, wameingiwa na hofu
kuu,
maana Mungu yupo pamoja na
wenye haki.
6 [l]Ninyi watenda mabaya
mnakwamisha mipango ya
maskini,
bali BWANA ndiye kimbilio lao.

7 [m]Laiti wokovu wa Israeli
ungalikuja kutoka Sayuni!
Wakati BWANA arejeshapo
wafungwa wa watu wake,
Yakobo na ashangilie,
Israeli na afurahi!

[h]**14:1** Za 10:4; Mwa 6:12; Rum 3:10; Mit 1:7, 22
[i]**14:2** Ay 41:34; Za 32:6; 85:11; 102:19; Ezr 6:21; Mao 3:50
[j]**14:3** 1Sam 8:3; 2Pet 2:7; 1Tim 5:15; 1Fal 8:46; Za 143:2; Mhu 7:20; Rum 3:10-12
[k]**14:4** Za 17:2; 82:5; 79:6; Mik 3:3; Isa 64:7; 65:1; Yer 4:22; 10:25; Hos 7:7
[l]**14:6** 2Sam 22:3
[m]**14:7** Za 2:6; Yer 48:47; Kum 30:3

## Zaburi 15

*Kitu Mungu Anachotaka*

*Zaburi ya Daudi.*

1 [a]BWANA, ni nani awezaye kukaa
katika Hekalu lako?
Nani awezaye kuishi
katika mlima wako mtakatifu?

2 [b]Ni yule aendaye pasipo mawaa,
atendaye yaliyo haki,
asemaye kweli toka moyoni mwake,
3 [c]na hana masingizio ulimini
mwake,
asiyemtenda jirani yake vibaya,
na asiyemsingizia mwenzake,
4 [d]ambaye humdharau mtu mbaya,
lakini huwaheshimu wale
wamwogopao BWANA,
yule atunzaye kiapo chake
hata kama anaumia.
5 [e]Yeye akopeshaye fedha yake bila
riba,
na hapokei rushwa dhidi ya mtu
asiye na hatia.

Mtu afanyaye haya
kamwe hatatikisika.

## Zaburi 16

*Sala Ya Matumaini*

*Utenzi wa Daudi.*

1 [f]Ee Mungu, uniweke salama,
kwa maana kwako nimekimbilia.

2 [g]Nilimwambia BWANA, "Wewe
ndiwe Bwana wangu;
pasipo wewe sina jambo jema."
3 [h]Kwa habari ya watakatifu walioko
duniani,
ndio walio wa fahari ambao
ninapendezwa nao.
4 [i]Huzuni itaongezeka kwa wale
wanaokimbilia miungu mingine.
Sitazimimina sadaka zao za damu
au kutaja majina yao midomoni
mwangu.

5 [j]BWANA umeniwekea fungu langu na
kikombe changu;
umeyafanya mambo yangu yote
yawe salama.
6 [k]Alama za mipaka zimeniangukia
mahali pazuri,
hakika nimepata urithi mzuri.

7 [l]Nitamsifu BWANA ambaye
hunishauri,
hata wakati wa usiku moyo wangu
hunifundisha.
8 [mn]Nimemweka BWANA mbele yangu
daima.
Kwa sababu yuko mkono wangu
wa kuume,
sitatikisika.

9 [o]Kwa hiyo moyo wangu unafurahia,
na ulimi wangu unashangilia;
mwili wangu nao utapumzika
salama,
10 [p]kwa maana hutaniacha kaburini,
wala hutamwacha Mtakatifu Wako
kuona uharibifu.

---

[a]**15:1** Za 27:4; 23:6; 2:5; 61:4; 20:2; 78:69; 150:1; Kut 29:46; 25:8; 15:17; 1Nya 22:19
[b]**15:2** 1The 3:13; Tit 1:6; Mit 16:13; Rum 9:1; Isa 38:15, 16; 45:19; Yer 7:28; 9:5; Mwa 6:9; Efe 1:4; 4:25; Za 18:32; 84:11; Zek 8:3, 16
[c]**15:3** Law 19:16
[d]**15:4** Ay 19:9; Yos 9:18; Mdo 28:10; Kum 23:21; Mt 5:33
[e]**15:5** Kut 22:25; 18:21; Mdo 24:26; 2Pet 1:10; Za 21:7; 112:6; Ay 29:18; Ebr 12:28
[f]**16:1** Za 25:20; 12:7; 2:12
[g]**16:2** Za 31:14; 73:25; 118:28; 140:6
[h]**16:3** Kum 33:3; Rum 1:7; Dan 7:18; Mdo 9:13; Za 30:4; 85:8; 101:6
[i]**16:4** Za 32:10; Kut 13:13; 18:11; 20:3; Mit 23:29; Kum 18:19; 31:20
[j]**16:5** Law 2:2; Za 23:5; 75:8; 116:13; Isa 51:17; Hab 2:16; Ay 22:26; Mao 4:21
[k]**16:6** Kum 19:14; Za 104:9; Ay 22:26; Mit 8:29; Yer 5:22
[l]**16:7** Za 73:24; 42:8; 77:6; Mit 15:22; Isa 11:2; Ay 35:10
[m]**16:8** Isa 36:15; 37:20
[n]**16:8** 1Fal 2:19; 1Nya 6:39; Za 73:23; 15:5
[o]**16:9** Za 4:7; 13:5; 28:7; 30:11; Kum 33:26
[p]**16:10** Za 30:3; 31:17; 49:15; 86:13; Mdo 2:27, 31; 13:35; Hos 13:14; 2Fal 19:22; Lk 1:35; Ay 17:14; Dan 9:24; Hes 16:30

11 [a]Umenijulisha njia ya uzima;
utanijaza na furaha mbele zako,
pamoja na furaha za milele
katika mkono wako wa kuume.

## Zaburi 17

*Sala Ya Mtu Asiye Na Hatia*

*Sala ya Daudi.*

1 [b]Sikia, Ee BWANA, kusihi kwangu
kwa haki,
sikiliza kilio changu.
Tega sikio kwa ombi langu,
halitoki kwenye midomo ya
udanganyifu.
2 [c]Hukumu yangu na itoke kwako,
macho yako na yaone yale yaliyo
haki.

3 [d]Ingawa unauchunguza moyo wangu
na kunikagua usiku,
ingawa umenijaribu, hutaona
chochote.
Nimeamua kwamba kinywa changu
hakitatenda dhambi.
4 [e]Kuhusu matendo ya wanadamu:
kwa neno la midomo yako,
nimejiepusha
na njia za wenye jeuri.
5 [f]Hatua zangu zimeshikamana na njia
zako;
nyayo zangu hazikuteleza.

6 [g]Ee Mungu, ninakuita, kwa kuwa
utanijibu,
nitegee sikio lako na usikie ombi
langu.
7 [h]Uonyeshe ajabu ya upendo wako
mkuu,
wewe uokoaye kwa mkono wako
wa kuume
wale wanaokukimbilia kutokana
na adui zao.
8 [i]Nilinde kama mboni ya jicho lako,
unifiche chini ya kivuli cha
mbawa zako
9 [j]kutokana na waovu
wanaonishambulia,
kutokana na adui wauaji
wanaonizunguka.

10 [k]Huifunga mioyo yao iliyo migumu,
vinywa vyao hunena kwa
majivuno.
11 [l]Wamenifuatia nyayo zangu, sasa
wamenizingira,
wakiwa macho, waniangushe
chini.
12 [m]Wamefanana na simba mwenye njaa
awindaye,
kama simba mkubwa anyemeleaye
mafichoni.

13 [n]Inuka, Ee BWANA, pambana nao,
uwaangushe,
niokoe kutokana na waovu kwa
upanga wako.
14 [o]Ee BWANA, mkono wako uniokoe na
watu wa jinsi hii,
kutokana na watu wa ulimwengu
huu
ambao fungu lao liko katika
maisha haya.

---

[a]**16:11** Mdo 2:25-28; Mt 7:14; Isa 29:13; Za 139:24; 21:6; 80:1, 17; 30:10; 64:1; 140:6; 5:1, 2; 39:12; 142:6
[b]**17:1** Za 30:10; 64:1; 80:1; 140:6; 5:1, 2; 39:12; 142:6; 143:1; Isa 29:13
[c]**17:2** Za 24:5; 26:1; 99:4; Isa 46:13; 50:8-9; 54:17
[d]**17:3** Za 139:1; Yak 3:2; Ay 7:18; 23:10; Yer 12:3; 50:20
[e]**17:4** Rum 12:2
[f]**17:5** Ay 23:11; Za 44:18; 73:2; 121:3; Kum 32:35
[g]**17:6** Za 84:7; 116:2; 4:1
[h]**17:7** Za 31:21; 69:13; 106:45; 107:43; 117:2; 10:12; 2:12
[i]**17:8** Hes 6:24; Isa 34:15; Kum 32:10; Mit 7:2; Za 27:5; 31:20; 32:7; 36:7; 63:7; Rum 2:12
[j]**17:9** Za 109:3
[k]**17:10** Za 73:7; 119:70; Isa 6:10; 2:3
[l]**17:11** Za 88:17; 1Sam 23:26
[m]**17:12** Za 7:2; Yer 5:6; 12:8; Mao 3:10; Mwa 49:9
[n]**17:13** Za 35:8; 55:23; 73:18; Hes 10:3
[o]**17:14** Za 49:17; Lk 16:8, 25; Isa 2:7; 57:17

Na wapate adhabu ya kuwatosha.
Watoto wao na wapate zaidi ya hayo,
hukumu na iendelee kwa watoto wa watoto wao.
15 [a]Na mimi katika haki nitauona uso wako,
niamkapo, nitaridhika kwa kuona sura yako.

### Zaburi 18

*Wimbo Wa Daudi Wa Ushindi*

**(2 Samweli 22:1-51)**

*Kwa mwimbishaji. Zaburi ya Daudi mtumishi wa Bwana aliyomwimbia Bwana wakati Bwana alipomwokoa mikononi mwa adui zake wote, na pia mkononi mwa Sauli. Alisema hivi:*

1 [b]Nakupenda wewe, Ee Bwana,
nguvu yangu.

2 [c]Bwana ni mwamba wangu,
ngome yangu na mwokozi wangu,
Mungu wangu ni mwamba,
ambaye kwake ninakimbilia.
Yeye ni ngao yangu na pembe ya wokovu wangu,
ngome yangu.
3 [d]Ninamwita Bwana anayestahili kusifiwa,
nami ninaokolewa kutoka kwa adui zangu.

4 [e]Kamba za mauti zilinizunguka,
mafuriko ya maangamizi yalinilemea.
5 [f]Kamba za kuzimu zilinizunguka,
mitego ya mauti ilinikabili.
6 [g]Katika shida yangu nalimwita Bwana,
nilimlilia Mungu wangu anisaidie.
Kutoka hekaluni mwake alisikia sauti yangu,
kilio changu kikafika mbele zake, masikioni mwake.

7 [h]Dunia ilitetemeka na kutikisika,
misingi ya milima ikatikisika,
vilitetemeka kwa sababu alikuwa amekasirika.
8 [i]Moshi ukapanda kutoka puani mwake,
moto uteketezao ukatoka kinywani mwake,
makaa ya moto yawakayo
yakatoka ndani mwake.
9 [j]Akazipasua mbingu akashuka chini,
mawingu meusi yalikuwa chini ya miguu yake.
10 [k]Alipanda juu ya kerubi akaruka,
akapaa juu kwa mbawa za upepo.
11 [l]Alifanya giza kuwa kitu chake cha kujifunika,
hema lake kumzunguka,
mawingu meusi ya mvua ya angani.
12 [m]Kutokana na mwanga wa uwepo wake
mawingu yalisogea,
ikanyesha mvua ya mawe
na umeme wa radi.
13 [n]Bwana alinguruma kutoka mbinguni,
sauti ya Aliye Juu Sana ilisikika.

---

[a]**17:15** Za 3:5; Hes 12:2; Mt 5:8; 1Yn 3:2
[b]**18:1** Kut 15:2; Yer 16:19; Kum 32:4; 33:29; Za 91:2; 22:19; 59:9; 81:1; 1Sam 2:2; Isa 2:10; 12:2; 49:5
[c]**18:2** Kut 33:22; Isa 2:1; 17:10; Yer 16:19; Za 40:17; 114:2; 2:12; 9:9; 94:20; 28:7, 8; 31:2, 3; 84:9; 119:114; Ebr 2:13; Mwa 15:1; Lk 1:69
[d]**18:3** 1Nya 16:25; Za 9:13; 76:4
[e]**18:4** Za 116:4; 93:4; 124:6; Eze 43:2; Isa 5:30; 17:12; Yer 6:23; 51:42, 55
[f]**18:5** Mit 14:13
[g]**18:6** Kum 4:30; Za 30:2; 99:6; 102; 120:1; 66:19; 116:1; Ay 16:18
[h]**18:7** Za 97:4; Isa 5:25; 64:3; Amu 5:4, 5; Ay 9:5; Yer 10:10; Mdo 4:31
[i]**18:8** Ay 41:20, 21; Kut 15:17; 19:18; Mit 25:22; Za 50:3; 97:3; Dan 7:10; Rum 12:20
[j]**18:9** Mwa 11:5; Isa 64:1; Za 57:3; 104:3; Kut 20:21; Kum 33:26
[k]**18:10** Mwa 3:24; Eze 10:18; Kum 33:26; Za 104:3; 99:1
[l]**18:11** Za 97:2; Kut 19:9; Ay 22:14; Isa 4:5; Kum 4:11; Yer 43:10
[m]**18:12** Za 104:2; Yos 10:10; Ay 36:30
[n]**18:13** Kut 9:23; Za 29:3; 2Sam 2:10

[14] [a]Aliipiga mishale yake na kutawanya adui,
naam, umeme mwingi wa radi na kuwafukuza.
[15] [b]Mabonde ya bahari yalifunuliwa,
na misingi ya dunia ikawa wazi
kwa kukaripia kwako, Ee BWANA,
kwa uvumi wa pumzi kutoka puani mwako.

[16] [c]Alinyoosha mkono kutoka juu na kunishika;
alinitoa kutoka kilindi cha maji makuu.
[17] [d]Aliniokoa kutoka adui wangu mwenye nguvu nyingi,
kutoka adui zangu waliokuwa na nguvu nyingi kuliko mimi.
[18] [e]Walinikabili siku ya msiba wangu,
lakini BWANA alikuwa msaada wangu.
[19] [f]Alinileta nje mahali penye nafasi tele,
akaniokoa kwa kuwa alipendezwa nami.

[20] [g]BWANA alinitendea sawasawa na uadilifu wangu;
sawasawa na usafi wa mikono yangu amenilipa.
[21] [h]Kwa maana nimezishika njia za BWANA;
sijatenda ubaya nikamwacha Mungu wangu.
[22] [i]Sheria zake zote zi mbele yangu,
wala sijayaacha maagizo yake.
[23] [j]Nimekuwa sina hatia mbele zake,
nami nimejilinda nisitende dhambi.
[24] [k]BWANA amenilipa sawasawa na uadilifu wangu;
sawasawa na usafi wa mikono yangu machoni pake.

[25] [l]Kwa yeye aliye mwaminifu, unajionyesha kuwa mwaminifu,
kwa asiye na hatia, unajionyesha kutokuwa na hatia.
[26] [m]Kwa aliye mtakatifu, unajionyesha kuwa mtakatifu,
lakini kwa aliyepotoka, unajionyesha kuwa mkaidi.
[27] [n]Wewe huwaokoa wanyenyekevu,
lakini huwashusha wenye kiburi.
[28] [o]Wewe, Ee BWANA, unaifanya taa yangu iendelee kuwaka;
Mungu wangu hulifanya giza langu kuwa mwanga.
[29] [p]Kwa msaada wako naweza kushinda jeshi,
nikiwa pamoja na Mungu wangu
nitaweza kuruka ukuta.

[30] [q]Kuhusu Mungu, njia yake ni kamilifu,
neno la BWANA halina dosari.
Yeye ni ngao kwa wote
wanaokimbilia kwake.

---

[a]**18:14** Kum 32:23; Ay 6:4; 36:30; Ufu 4:5; Za 21:12; Amu 4:15; Hes 24:8
[b]**18:15** Za 11:3; 76:6; 104:7; 106:9; Isa 50:2; Kut 15:8
[c]**18:16** Kut 15:5; Mit 18:4; 20:5; Za 69:2; 144:7
[d]**18:17** Za 38:19; 59:1; 143:9; Amu 18:26
[e]**18:18** Mit 1:27; 16:4; Yer 17:17; 40:2; Oba 1:13; Za 20:2; Isa 3:1
[f]**18:19** Za 31:8; 118:5; Hes 14:8
[g]**18:20** 1Sam 22:21; 26:23; Ay 22:30; Za 24:4; Rum 2:12; 2Nya 15:7; 1Kor 3:8; Mit 6:4
[h]**18:21** 2Nya 34:33; Za 37:34; 119:2; 102; Mit 8:32; 23:26
[i]**18:22** Za 119:30
[j]**18:23** Mwa 6:9
[k]**18:24** 1Sam 26:23; Rut 2:12; Mt 10:41-42
[l]**18:25** Za 31:23; 37:23; 50:5; 25:10; 40:11; 89:24; 146:6; Mit 2:8; Mt 18:32-35
[m]**18:26** Mit 15:26; Mt 5:8; Flp 1:10; 1Tim 5:22; Tit 1:15; 1Yn 3:3; Mit 3:34; Mt 10:16; Lk 16:8; Law 26:23
[n]**18:27** 2Nya 33:23; Mt 23:12; Ay 41:34; Za 10:5; Mit 3:33-35; 6:17
[o]**18:28** 1Fal 11:36; Za 132:17; Ay 29:3; Za 97:11; 112:4; Yn 1:5; Mdo 26:18; 2Kor 4:6; 2Pet 1:19; Ay 18:6
[p]**18:29** Isa 45:5; Ebr 11:34
[q]**18:30** Kum 32:4; Za 12:6; 3:3; 2:12; Mit 30:5; Ufu 15:3; Rum 12:3

31 [a]Kwa maana ni nani aliye Mungu
zaidi ya BWANA?
Ni nani aliye Mwamba
isipokuwa Mungu wetu?
32 [b]Mungu ndiye anivikaye nguvu
na kufanya njia yangu kuwa
kamilifu.
33 [c]Huifanya miguu yangu kama miguu
ya kulungu,
huniwezesha kusimama mahali
palipo juu.
34 [d]Huifundisha mikono yangu kupigana
vita;
mikono yangu inaweza kupinda
upinde wa shaba.
35 [e]Hunipa ngao yako ya ushindi,
nao mkono wako wa kuume
hunitegemeza,
unajishusha chini ili kuniinua.
36 [f]Huyapanua mapito yangu,
ili miguu yangu isiteleze.

37 [g]Niliwafuatia adui zangu na
nikawapata,
sikurudi nyuma mpaka
walipoangamizwa.
38 [h]Niliwaseta hata hawakuweza
kuinuka tena;
walianguka chini ya miguu yangu.
39 [i]Ulinivika nguvu kwa ajili ya
kupigana vita;
uliwafanya adui zangu wasujudu
miguuni pangu.
40 [j]Uliwafanya adui zangu wageuke na
kukimbia,
nami nikawaangamiza adui zangu.
41 [k]Walipiga yowe, lakini hapakuwepo
na yeyote wa kuwaokoa;
walimlilia BWANA, lakini
hakuwajibu.
42 [l]Niliwaponda kama mavumbi
yanayopeperushwa na upepo;
niliwamwaga nje kama tope
barabarani.

43 [m]Umeniokoa kutokana na
mashambulizi ya watu;
umenifanya kuwa kiongozi wa
mataifa,
watu ambao sikuwajua
wananitumikia.
44 [n]Mara wanisikiapo hunitii,
wageni hunyenyekea mbele
yangu.
45 [o]Wote wanalegea,
wanatoka katika ngome zao
wakitetemeka.

46 [p]BWANA yu hai! Sifa ni kwa
Mwamba wangu!
Atukuzwe Mungu Mwokozi
wangu!
47 [q]Yeye ndiye Mungu anilipiziaye
kisasi,
awatiishaye mataifa chini yangu,
48 [r]aniokoaye na adui zangu.
Uliniinua juu ya adui zangu;
uliniokoa toka kwa watu wajeuri.

---

[a]**18:31** Kum 4:5; 32:39; Za 35:10; 86:8; 89:6; Isa 46:9; 44:6, 8; 45:5, 6, 14, 18, 21; Mwa 49:24
[b]**18:32** 1Pet 5:10; Yak 3:2; Za 15:2; 19:13; Ebr 10:14
[c]**18:33** Za 42:1; Mit 5:19; Isa 35:6; Hab 3:19; Kum 32:13
[d]**18:34** Za 144:1
[e]**18:35** Za 3:5; 37:5, 17; 41:3; 51:2; 54:4; 55:22; 119:116; Isa 41:4, 10, 13; 43:2; 46:4
[f]**18:36** Ay 18:7; Za 31:8; 66:9
[g]**18:37** Law 26:7
[h]**18:38** Za 68:21; 110:6; 36:12; 47:3; 140:10; Isa 26:14
[i]**18:39** Za 18:32, 47; Isa 45:5, 24; Za 47:3; 144:2
[j]**18:40** Yos 7:12; Za 18:37
[k]**18:41** 2Fal 14:26; Za 50:22; 1Sam 8:18; 14:37; Yer 11:11; Mit 1:28
[l]**18:42** Kum 9:21; Isa 2:22
[m]**18:43** 2Sam 8:1-14; Isa 55:5
[n]**18:44** Za 144:7, 11; 54:3; Isa 25:5
[o]**18:45** 2Kor 4:1; Ebr 12:3; 1Sam 17:32; Isa 66:2; Hos 3:5; 11:10; Za 9:9; Mik 7:17
[p]**18:46** Yos 3:10; 2Kor 13:4; 1Sam 14:39; Kut 33:22; Za 21:13; 35:27; 40:16; 108:5; 1Nya 16:35; Lk 1:47; Yer 10:10
[q]**18:47** Mwa 4:24; Za 18:29; Amu 4:23
[r]**18:48** Dan 3:17; Za 7:10; 37:40; 140:2; 18:49

49 [a]Kwa hiyo nitakusifu katikati ya
mataifa, Ee BWANA;
nitaliimbia sifa jina lako.
50 [b]Humpa mfalme wake ushindi mkuu,
huonyesha fadhili zake kwa
mpakwa mafuta wake,
kwa Daudi na wazao wake milele.

## Zaburi 19

*Utukufu Wa Mungu Katika Uumbaji*

*Kwa mwimbishaji. Zaburi ya Daudi.*

1 [c]Mbingu zinatangaza utukufu wa
Mungu,
anga zahubiri kazi ya mikono
yake.
2 [d]Siku baada ya siku zinatoa habari,
usiku baada ya usiku zinatangaza
maarifa.
3 Hakuna msemo wala lugha,
ambapo sauti zao hazisikiki.
4 [e]Sauti yao imeenea duniani pote,
nayo maneno yao yameenea
hadi miisho ya ulimwengu.

Katika mbingu amepiga hema kwa
ajili ya jua,
5 [f]linafanana na bwana arusi
akitoka chumbani mwake,
kama shujaa afurahiavyo
kukamilisha kushindana kwake.
6 [g]Huchomoza upande mmoja wa
mbingu,
na kufanya mzunguko wake
hadi upande mwingine.
Hakuna kilichojificha joto lake.

7 [h]Sheria ya BWANA ni kamilifu,
ikihuisha nafsi.
Shuhuda za BWANA ni za kuaminika,
zikimpa mjinga hekima.
8 [i]Maagizo ya BWANA ni kamili,
nayo hufurahisha moyo.
Amri za BWANA huangaza,
zatia nuru machoni.
9 [j]Kumcha BWANA ni utakatifu,
nako kwadumu milele.
Amri za BWANA ni za hakika,
nazo zina haki.
10 [k]Ni za thamani kuliko dhahabu,
kuliko dhahabu iliyo safi sana,
ni tamu kuliko asali,
kuliko asali kutoka kwenye sega.
11 [l]Kwa hizo mtumishi wako
anaonywa,
katika kuzishika kuna thawabu
kubwa.

12 [m]Ni nani awezaye kutambua makosa
yake?
Nisamehe makosa yangu
nisiyoyajua.
13 [n]Mlinde mtumishi wako na dhambi
za makusudi,
nazo zisinitawale.
Ndipo nitakapokuwa sina lawama,
wala sitakuwa na hatia ya kosa
kubwa.

14 [o]Maneno ya kinywa changu
na mawazo ya moyo wangu,
yapate kibali mbele zako, Ee
BWANA,
Mwamba wangu na Mkombozi
wangu.

---

[a]**18:49** Za 101:1; 7:17; 9:2; 108:1; 146:2; Rum 15:9
[b]**18:50** 2Sam 23:1; Za 144:10; 89:4
[c]**19:1** Isa 6:3; 40:22; Za 4:2; 97:6; 89:5; 50:6; 8:1, 6; 148:3; 103:22; Rum 1:19; Mwa 1:8
[d]**19:2** Za 74:16
[e]**19:4** Rum 10:18; Za 104:2; Ay 36:29; Amu 5:31
[f]**19:5** 1Sam 17:4; Mhu 11:7; Yoe 2:16; Ay 36:29
[g]**19:6** Kum 30:4; Za 11:3; Mhu 1:5
[h]**19:7** Yak 1:25; Kum 4:6; Za 1:2; 23:3; 93:5; 119:130, 138, 142, 144; 11:7
[i]**19:8** Za 33:4; 38:10; 119:14, 128; Ezr 9:7; Neh 9:13; Rum 7:12
[j]**19:9** Mhu 12:13; Isa 33:6; Za 34:11; 111:10; 119:138; Mit 1:7
[k]**19:10** Ay 22:24; Eze 3:3; Mit 8:10; 1Sam 14:27; Za 119:72, 103
[l]**19:11** Mit 6:22
[m]**19:12** Za 51:2; 90:8; Mhu 12:14
[n]**19:13** Hes 15:30; Mwa 6:9; Za 18:32; 119:133
[o]**19:14** Za 104:34; 18:31; Kut 6:6; Isa 44:6; Ay 19:25

### Zaburi 20

*Maombi Kwa Ajili Ya Ushindi*

*Kwa mwimbishaji. Zaburi ya Daudi.*

1 [a]BWANA na akujibu unapokuwa
katika dhiki,
jina la Mungu wa Yakobo na liwe
kinga yako.
2 [b]Na akutumie msaada kutoka
patakatifu
na akupatie msaada kutoka
Sayuni.
3 [c]Na azikumbuke dhabihu zako zote,
na azikubali sadaka zako za
kuteketezwa.
4 [d]Na akujalie haja ya moyo wako,
na aifanikishe mipango yako yote.
5 [e]Tutashangilia kwa furaha
utakaposhinda,
tutainua bendera zetu kwa jina la
Mungu wetu.
BWANA na akupe haja zako zote.

6 [f]Sasa nafahamu kuwa BWANA
humwokoa mpakwa mafuta wake,
humjibu kutoka mbingu yake
takatifu
kwa nguvu za wokovu wa mkono
wake wa kuume.
7 [g]Wengine wanatumaini magari ya
vita, na wengine farasi,
bali sisi tutalitumainia jina la
BWANA, Mungu wetu.
8 [h]Wao wameshushwa chini na
kuanguka,
bali sisi tunainuka na kusimama
imara.

9 [i]Ee BWANA, mwokoe mfalme!
Tujibu tunapokuita!

### Zaburi 21

*Shukrani Kwa Mungu Kwa Ajili Ya Ushindi*

*Kwa mwimbishaji. Zaburi ya Daudi.*

1 [j]Ee BWANA, mfalme huzifurahia
nguvu zako.
Tazama jinsi ilivyo kuu furaha
yake
kwa ushindi unaompa!
2 [k]Umempa haja ya moyo wake
na hukumzuilia maombi ya
midomo yake.
3 [l]Ulimkaribisha kwa baraka tele
na kumvika taji ya dhahabu safi
kichwani pake.
4 [m]Alikuomba maisha, nawe ukampa,
wingi wa siku milele na milele.
5 [n]Kutokana na ushindi uliompa,
utukufu wake ni mkubwa,
umeweka juu yake fahari na
utukufu.
6 [o]Hakika umempa baraka za milele,
umemfanya awe na furaha
kwa shangwe ya uwepo wako.
7 [p]Kwa kuwa mfalme anamtumaini
BWANA;
kwa upendo usiokoma wa Aliye
Juu Sana hatatikiswa.

---

[a]**20:1** Za 4:1; 46:7; 59:1; 69:29; 91:14; Kut 3:6; Isa 50:10
[b]**20:2** Hes 3:28; Za 2:6; 30:10; 33:20; 37:40; 40:17; 54:4; 128:5; 18:18; 134:3; 135:21
[c]**20:3** Mdo 10:4; Kum 33:11
[d]**20:4** Za 21:2; 37:4; 140:8; 145:16, 19; Isa 26:8; Eze 24:25; Rum 10:1; Mit 16:3; Dan 11:17; 1Yn 5:14, 15
[e]**20:5** Hes 1:52; Isa 5:26; 11:10, 12; 13:2; 30:17; 49:22; 62:10; Yer 50:2; 51:12, 27; Ay 3:7; 1Sam 1:17; 12:1, 2; 17:45; Za 60:4
[f]**20:6** 2Sam 23:1; Ay 40:14; Za 28:8; Hab 3:13
[g]**20:7** 2Fal 19:23; Za 33:17; 147:10; Mit 21:31; Isa 31:1; 36:8, 9; 2Nya 32:8; Kum 17:16; Amu 7:7
[h]**20:8** Za 27:2; 37:23; Isa 7:9; 40:30; Yer 46:6; 50:32; Mik 7:8; Ay 11:15; Mit 10:25
[i]**20:9** Za 17:6
[j]**21:1** 1Sam 2:10; 2Sam 22:51
[k]**21:2** Za 20:4; Yn 11:42
[l]**21:3** 2Sam 12:30; Ufu 14:14; Zek 6:11
[m]**21:4** Za 10:16; 45:17; 48:14; 133:3; 2Sam 7:19
[n]**21:5** Za 18:50; 44:4; 8:5; 45:3; 93:1; 96:6; 104:1
[o]**21:6** Za 43:4; 126:3; 1Nya 17:27
[p]**21:7** 2Fal 18:5; Za 6:4; 15:5; 55:22; 91:7; Mwa 14:18

8 [a]Mkono wako utawashika adui zako
wote,
mkono wako wa kuume
utawakamata adui zako.
9 [b]Wakati utakapojitokeza
utawafanya kama tanuru ya moto.
Katika ghadhabu yake BWANA
atawameza,
moto wake utawateketeza.
10 [c]Utawaangamiza wazao wao kutoka
duniani,
uzao wao kutoka wanadamu.
11 [d]Ingawa watapanga mabaya dhidi
yako
na kutunga hila, hawawezi
kufanikiwa,
12 [e]kwa kuwa utawafanya wakimbie
utakapowalenga usoni pao
kwa mshale kutoka kwenye
upinde wako.

13 [f]Ee BWANA, utukuzwe katika nguvu
zako,
tutaimba na kusifu nguvu zako.

## Zaburi 22

*Kilio Cha Uchungu Na Wimbo Wa Sifa*

*Kwa mwimbishaji. Mtindo wa utenzi wa "Kulungu wa Alfajiri." Zaburi ya Daudi.*

1 [g]Mungu wangu, Mungu wangu,
mbona umeniacha?
Kwa nini uko mbali hivyo
kuniokoa?
Mbali hivyo na maneno ya kuugua
kwangu?
2 [h]Ee Mungu wangu, ninalia mchana,
lakini hunijibu,
hata usiku, sinyamazi.
3 [i]Hata hivyo umesimikwa katika
kiti cha enzi kama Uliye
Mtakatifu;
wewe ni sifa ya Israeli.[j]
4 [k]Kwako wewe baba zetu waliweka
tumaini lao,
walikutumaini nawe ukawaokoa.
5 [l]Walikulilia wewe na ukawaokoa,
walikutegemea wewe nao
hawakuaibika.

6 [m]Mimi ni mnyoo wala si
mwanadamu,
wanaume wamenibeza, na watu
wamenidharau.
7 [n]Wote wanionao hunidhihaki,
hunivurumishia matusi, wakitikisa
vichwa vyao:
8 [o]Husema, "Anamtegemea BWANA,
basi BWANA na amwokoe.
Amkomboe basi, kwa maana
anapendezwa naye."

9 [p]Hata hivyo ulinitoa tumboni,
ukanifanya nikutegemee,
hata nilipokuwa ninanyonya
matiti ya mama yangu.
10 [q]Nimekabidhiwa kwako tangu
kuzaliwa,
toka tumboni mwa mama yangu
umekuwa Mungu wangu.

---

[a]**21:8** Isa 10:10
[b]**21:9** Kum 32:22; Yer 15:14
[c]**21:10** Kum 28:18
[d]**21:11** Za 2:1; 10:2; 26:10; 37:7; Ay 10:3
[e]**21:12** Kut 23:27
[f]**21:13** Za 18:46; Ufu 15:3, 4
[g]**22:1** Za 9:10; 10:1; Mt 27:46; Ay 3:24; 6:15; Mk 15:34; Ebr 5:7
[h]**22:2** Ay 19:7; Za 42:3; 88:1
[i]**22:3** 2Fal 19:22; Za 71:22; 148:14; Mk 1:24; Ufu 4:8; Kut 15:2; Isa 6:3
[j]3 Tafsiri zingine zinasema: uketiye juu ya sifa za Israeli.
[k]**22:4** Za 78:53; 107:6
[l]**22:5** 1Nya 5:20; Rum 9:33; Za 25:3; 31:17; 71:1; 2Nya 13:18; Isa 8:17; 25:9; 26:3; 30:18; 49:23
[m]**22:6** Ay 4:19; Mt 16:21; Mal 2:9; Isa 60:14; 49:7; 53:3; Za 119:141; 64:8; 109:25; 69:19; 2Sam 12:14
[n]**22:7** Mt 9:24; 27:41; Mk 15:20, 29, 31, 32; Lk 16:14; 23:36, 39; Mt 27:39, 44; Ay 17:2; Za 35:16; 69:12; 74:18
[o]**22:8** Za 91:14; 3:2; 2Sam 22:20; Mt 3:17; 27:43
[p]**22:9** Ay 10:18; Hes 1:7; Za 71:6; 78:7
[q]**22:10** Za 71:6; Isa 46:3; 49:1

11 [a]Usiwe mbali nami,
kwa maana shida iko karibu
na hakuna wa kunisaidia.

12 [b]Mafahali wengi wamenizunguka,
mafahali wa Bashani wenye nguvu
wamenizingira.
13 [c]Simba wangurumao wanaorarua
mawindo
yao hupanua vinywa vyao dhidi
yangu.
14 [d]Nimemiminwa kama maji,
mifupa yangu yote imetoka katika
viungo vyake.
Moyo wangu umegeuka kuwa nta,
umeyeyuka ndani yangu.
15 [e]Nguvu zangu zimekauka kama
kigae,
ulimi wangu umegandamana
na kaakaa la kinywa changu,
kwa sababu umenilaza
katika mavumbi ya kifo.
16 [f]Mbwa wamenizunguka,
kundi la watu waovu
limenizingira,
wametoboa mikono yangu na
miguu yangu.
17 [g]Naweza kuhesabu mifupa yangu
yote,
watu wananikodolea macho na
kunisimanga.
18 [h]Wanagawana nguo zangu wao kwa
wao,
na vazi langu wanalipigia kura.

19 [i]Lakini wewe, Ee Bwana,
usiwe mbali.
Ee Nguvu yangu,
uje haraka unisaidie.
20 [j]Okoa maisha yangu na upanga,
uhai wangu wa thamani kutoka
nguvu za mbwa.
21 [k]Niokoe kutoka kinywani mwa
simba,
niokoe kutoka pembe za mafahali
mwitu.

22 [l]Nitalitangaza jina lako kwa ndugu
zangu,
katika kusanyiko nitakusifu wewe.
23 [m]Ninyi ambao mnamcha Bwana,
msifuni!
Ninyi nyote wazao wote wa
Yakobo, mheshimuni yeye!
Mcheni yeye, ninyi wazao wote
wa Israeli!
24 [n]Kwa maana hakupuuza wala
kudharau
mateso ya aliyeonewa;
hakumficha uso wake
bali alisikiliza kilio chake ili
amsaidie.

25 [o]Kwako wewe hutoka kiini cha
sifa zangu katika kusanyiko
kubwa,
nitatimiza nadhiri zangu mbele ya
wale wakuchao wewe.
26 [p]Maskini watakula na kushiba,
wale wamtafutao Bwana
watamsifu:
mioyo yenu na iishi milele!

---

[a]**22:11** Za 10:1, 14; 2Fal 14:26; Isa 41:28
[b]**22:12** Za 69:30; 17:9; 27:6; 49:5; 109:3; 140:9; Kum 32:14; Isa 2:3; Eze 27:6; 39:18; Amo 4:1
[c]**22:13** Eze 22:25; Sef 3:3; Mwa 49:9; 1Pet 5:8; Mao 3:6; Za 35:21
[d]**22:14** Za 6:2
[e]**22:15** Isa 45:9; Yn 19:28; Za 137:6; 104:29; Mao 4:4; Ay 7:21; Eze 3:26
[f]**22:16** Flp 3:2; Isa 51:9; 53:5; Mit 17:22; Zek 12:10; Yn 20:25
[g]**22:17** Lk 23:35; Mik 7:8; Za 25:2; 30:1; 35:19; 38:16; Mao 2:17
[h]**22:18** Law 16:8; Yn 19:24; Mt 27:35; Mk 9:12; 15:24; Lk 23:34
[i]**22:19** Za 18:1; 38:22; 70:5; 14:1; 40:13
[j]**22:20** Ay 5:20; Za 141:1; 40:13
[k]**22:21** Ay 4:10, 12; Ebr 2:12; Hes 23:22; Za 22:13; 68:26; 40:9, 10; 35:18; 2Tim 4:17
[l]**22:22** Za 26:12; 35:18; 40:9, 10; 68:26; Ebr 2:12; Yn 20:17
[m]**22:23** Yer 3:17; Za 66:8; 33:2, 8; 103:1; 86:12; 106:1; 50:15; 113:1; 117:1; 135:19; Isa 24:15; 25:3; 49:23; 60:9; Kum 14:23
[n]**22:24** Ebr 5:7; Za 9:12; 102:17; 13:1; 27:9; 69:17; 102:2; 143:7; Ay 24:12; 36:5
[o]**22:25** Za 26:12; 35:18; 40:9; 82:1; Hes 30:2
[p]**22:26** Za 107:9; 40:16

27 [a]Miisho yote ya dunia itakumbuka
na kumgeukia BWANA,
nazo jamaa zote za mataifa
watasujudu mbele zake,
28 [b]kwa maana ufalme ni wa BWANA
naye hutawala juu ya mataifa.

29 [c]Matajiri wote wa dunia
watasherehekea na kuabudu.
Wote waendao mavumbini
watapiga magoti mbele yake,
wote ambao hawawezi
kudumisha uhai wao.
30 [d]Wazao wa baadaye watamtumikia
yeye;
vizazi vijavyo vitajulishwa habari
za Bwana.
31 [e]Watatangaza haki yake kwa watu
ambao hawajazaliwa bado,
kwa maana yeye ametenda hili.

## Zaburi 23

*BWANA Mchungaji Wetu*

*Zaburi ya Daudi.*

1 [f]BWANA ndiye mchungaji wangu,
sitapungukiwa na kitu.
2 [g]Hunilaza katika malisho
ya majani mabichi,
kando ya maji matulivu huniongoza,
3 [h]hunihuisha nafsi yangu.
Huniongoza katika njia za haki
kwa ajili ya jina lake.
4 [i]Hata kama nikipita katikati
ya bonde la uvuli wa mauti,
sitaogopa mabaya,
kwa maana wewe upo pamoja
nami;
fimbo yako na mkongojo wako
vyanifariji.

5 [j]Waandaa meza mbele yangu
machoni pa adui zangu.
Umenipaka mafuta kichwani pangu,
kikombe changu kinafurika.
6 [k]Hakika wema na upendo vitanifuata
siku zote za maisha yangu,
nami nitakaa nyumbani mwa
BWANA
milele.

## Zaburi 24

*Mfalme Mkuu*

*Zaburi ya Daudi.*

1 [l]Dunia ni mali ya BWANA, na vyote
vilivyomo ndani yake,
ulimwengu, na wote waishio ndani
yake,
2 [m]maana aliiwekea misingi yake
baharini
na kuifanya imara juu ya maji.

3 [n]Nani awezaye kuupanda mlima wa
BWANA?
Ni nani awezaye kusimama
patakatifu pake?
4 [o]Ni yule mwenye mikono safi na
moyo mweupe,
yule ambaye hakuinulia sanamu
nafsi yake
au kuapa kwa kitu cha uongo.
5 [p]Huyo atapokea baraka kutoka kwa
BWANA,
na hukumu ya haki kutoka kwa
Mungu Mwokozi wake.

---

[a]**22:27** Za 2:8; 86:9; 102:22; Dan 7:27; Mik 4:1
[b]**22:28** Za 47:7; Zek 14:9; Mt 6:13
[c]**22:29** Za 45:12; 89:48; 95:6; 96:9; 99:5; Isa 26:19; 27:13; 49:7; 66:23; Zek 14:16
[d]**22:30** Isa 53:10; 54:3; 61:9; 66:22; Za 102:18
[e]**22:31** Za 5:8; 71:18; 78:6; 40:9; 102:18; Lk 18:31; 24:44
[f]**23:1** Mwa 48:15; Yn 10:11; Flp 4:19; Za 28:9; 34:9, 10; 84:11; 107:9; 1Pet 2:25
[g]**23:2** Eze 34:14; Ufu 7:17; Za 36:8; 46:4
[h]**23:3** Isa 42:16; Za 5:8; 106:8; 19:7; 79:9; 25:9, 11; 73:24; 31:3; 109:21; 143:11
[i]**23:4** Ay 3:5; Za 107:14; Isa 43:2; Za 3:6; 27:1; 16:8; 46:11; Isa 8:10; Zek 8:23; Mt 1:23; Mdo 18:9, 10
[j]**23:5** Ay 36:16; Za 16:5; 45:7; 92:10; Lk 7:46
[k]**23:6** Neh 9:25; 2Kor 5:1
[l]**24:1** Kut 9:29; Ay 41:11; 1Kor 10:26
[m]**24:2** Za 104:3; Mwa 1:6; 2Pet 3:5
[n]**24:3** Za 2:6; 15:1; 65:4
[o]**24:4** 2Sam 22:21; Za 51:10; 73:1; Mt 5:8; Eze 18:15
[p]**24:5** Kum 11:26; Za 17:2

6 [a]Hiki ndicho kizazi cha wale
wamtafutao,
wale wautafutao uso wako, Ee
Mungu wa Yakobo.

7 [b]Inueni vichwa vyenu, enyi malango,
inukeni enyi milango ya kale,
ili mfalme wa utukufu apate
kuingia.
8 [c]Ni nani huyu Mfalme wa utukufu?
Ni BWANA aliye na nguvu na
uweza,
ni BWANA aliye hodari katika vita.
9 Inueni vichwa vyenu, enyi malango,
viinueni juu enyi milango ya kale,
ili Mfalme wa utukufu apate
kuingia.
10 [d]Ni nani yeye, huyu Mfalme wa
utukufu?
Ni BWANA Mwenye Nguvu Zote;
yeye ndiye Mfalme wa utukufu.

## Zaburi 25[e]

*Kumwomba Mungu Uongozi Na Ulinzi*

*Zaburi ya Daudi.*

1 [f]Kwako wewe, Ee BWANA,
nainua nafsi yangu,
2 [g]ni wewe ninayekutumainia,
Ee Mungu wangu.
Usiniache niaibike,
wala usiache adui zangu
wakanishinda.
3 [h]Kamwe hakuna hata mmoja
anayekutegemea
atakayeaibishwa,
bali wataaibishwa
wafanyao hila bila sababu.
4 [i]Nionyeshe njia zako, Ee BWANA,
nifundishe mapito yako,
5 [j]niongoze katika kweli yako na
kunifundisha,
kwa maana wewe ni Mungu
Mwokozi wangu,
nalo tumaini langu liko kwako
wakati wote.
6 [k]Kumbuka, Ee BWANA, rehema zako
kuu na upendo,
kwa maana zimekuwepo tangu
zamani.
7 [l]Usizikumbuke dhambi za ujana
wangu
wala njia zangu za uasi,
sawasawa na upendo wako
unikumbuke,
kwa maana wewe ni mwema, Ee
BWANA.

8 [m]BWANA ni mwema na mwenye adili,
kwa hiyo huwafundisha wenye
dhambi njia zake.
9 [n]Huwaongoza wanyenyekevu katika
haki,
naye huwafundisha njia yake.
10 [o]Njia zote za BWANA ni za upendo na
uaminifu
kwa wale wanaoshika shuhuda za
agano lake.
11 [p]Ee BWANA, kwa ajili ya jina lako,
unisamehe uovu wangu,
ijapokuwa ni mwingi.
12 [q]Ni nani basi, mtu yule anayemcha
BWANA?
Atamfundisha katika njia
atakayoichagua kwa ajili yake.

---

[a]**24:6** Za 27:8; 105:4; 119:58; Hos 5:15
[b]**24:7** Isa 26:2; 60:11, 18; 62:10; Za 74:12; 29:3; 118:19, 20; 44:4; Mdo 7:2; 1Kor 2:8; Zek 9:9; Mt 21:5; Hag 2:7; Mal 3:1
[c]**24:8** 1Nya 29:11; Za 89:13; Kum 4:34; Yer 50:34; Efe 6:10; Kut 15:3, 6
[d]**24:10** 1Sam 1:11
[e]Zaburi hii imetungwa kila mstari ukianzia na herufi ya alfabeti ya Kiebrania zikifuatana tangu Aleph (A) hadi Taw (T); zote ni 22.
[f]**25:1** Za 86:4; 143:8
[g]**25:2** Za 31:6; 143:8
[h]**25:3** Za 22:5; 2Tim 3:4; Isa 29:22; 24:16; Hab 1:13; Sef 3:4
[i]**25:4** Ay 34:32
[j]**25:5** Za 31:3; 43:3; Yn 16:13
[k]**25:6** Za 5:7; 98:3; Isa 63:7, 15; Yer 31:20; Hos 11:8
[l]**25:7** Ay 13:26; Isa 54:4; Yer 3:25; 31:19; 32:30; 2Tim 2:22; Eze 16:22, 60; 23:3; Za 34:8; 83:1; 107:17; 6:4; 51:1; 69:16; 109:26; 119:124; Kut 3:21; 1Nya 16:34
[m]**25:8** Za 32:8; 92:15; Isa 26:7; 28:26
[n]**25:9** Za 23:3, 4; 18:25; 103:18; 132:12
[o]**25:10** Za 18:25; 103:18; 132:12
[p]**25:11** Kut 9:16; Za 31:3; 79:9; 34:9; Kut 32:30; Za 78:38; Yer 14:7
[q]**25:12** Ay 1:8

13 [a]Mtu huyo atafanikiwa maishani
mwake,
nao wazao wake watairithi nchi.
14 [b]Siri ya BWANA iko kwa wale
wamchao,
yeye huwajulisha agano lake.
15 [c]Macho yangu humwelekea BWANA
daima,
kwa kuwa yeye peke yake ndiye
ataitoa
miguu yangu kutoka mtego.

16 [d]Nigeukie na unihurumie,
kwa maana mimi ni mpweke na
mwenye kuteseka.
17 [e]Shida za moyo wangu
zimeongezeka,
niokoe katika dhiki yangu.
18 [f]Uangalie mateso na shida zangu
na uniondolee dhambi zangu zote.
19 [g]Tazama adui zangu walivyo wengi,
pia uone jinsi wanavyonichukia
vikali!
20 [h]Uyalinde maisha yangu na uniokoe,
usiniache niaibike,
kwa maana nimekukimbilia wewe.
21 [i]Uadilifu na uaminifu vinilinde,
kwa sababu tumaini langu ni
kwako.

22 [j]Ee Mungu, wakomboe Israeli,
katika shida zao zote!

## Zaburi 26

*Maombi Ya Mtu Mwema*

*Zaburi ya Daudi.*

1 [k]Ee BWANA, nithibitishe katika haki,
maana nimeishi maisha yasiyo na
lawama;
nimemtumainia BWANA
bila kusitasita.
2 [l]Ee BWANA, unijaribu, unipime,
uuchunguze moyo wangu
na mawazo yangu;
3 [m]kwa maana upendo wako
uko mbele yangu daima,
nami natembea siku zote
katika kweli yako.
4 [no]Siketi pamoja na watu
wadanganyifu,
wala siandamani na wanafiki,
5 [p]ninachukia kusanyiko la watenda
mabaya
na ninakataa kuketi pamoja na
waovu.
6 [q]Ninanawa mikono yangu kwa kuwa
sina hatia,
naikaribia madhabahu yako, Ee
BWANA,
7 [r]nikitangaza sifa yako kwa sauti
kubwa,
huku nikisimulia matendo yako ya
ajabu.
8 [s]Ee BWANA, naipenda nyumba yako
mahali unakoishi,
mahali ambapo utukufu wako
hukaa.

---

[a]**25:13** Kum 30:15; Mt 5:5; Ay 8:7; 1Fal 3:14; Hes 14:24
[b]**25:14** Mit 3:32; Yn 7:17; Mwa 17:2
[c]**25:15** 2Nya 20:12; Za 119:110; 123:2; Ebr 12:2; Ay 34:30
[d]**25:16** Hes 6:25; Za 6:4; 68:6
[e]**25:17** 1Fal 1:29; Za 6:3; 39:2; 34:6, 17; 40:12; 54:7; 116:3
[f]**25:18** Za 13:3; Rum 12:12; 2Sam 16:12
[g]**25:19** Za 3:1; 9:13; 69:4; 35:19
[h]**25:20** Za 2:12; 86:2; 17:13; 22:21; 43:1; 71:2; 116:4; 140:1; 142:6; 144:11
[i]**25:21** Mwa 20:5; Mal 2:6; Mit 10:9; 1Fal 9:4; Za 88:10; 111:8; Isa 60:17
[j]**25:22** Za 103:8; Lk 24:21

[k]**26:1** 1Sam 24:15; Isa 12:2; 25:9; Mit 20:7; Yer 17:7; Za 15:2; 22:4; 40:4; 2Fal 20:3; Dan 3:28; Ebr 10:23
[l]**26:2** Za 7:9; 66:10; Kum 6:6; Eze 11:5; Yer 22:20; 20:12
[m]**26:3** 1Fal 2:4; Za 6:4; 40:11; 43:3; 86:11; 119:30
[n]**26:4** Za 1:1; 28:3; Mt 6:2
[o]**26:4** Amo 9:6; Zek 10:1
[p]**26:5** Za 139:21
[q]**26:6** Za 73:13; Mt 27:24
[r]**26:7** Isa 42:12; 60:6; Yos 3:5; Za 9:1
[s]**26:8** Za 96:6; 122:6; Isa 66:10; 2Nya 7:1; Kut 29:43

9 [a]Usiiondoe nafsi yangu pamoja na
watenda dhambi,
wala uhai wangu pamoja na
wamwagao damu,
10 [b]ambao mikononi mwao kuna
mipango miovu,
ambao mikono yao ya kuume
imejaa rushwa.
11 [c]Bali mimi ninaishi maisha yasiyo na
lawama;
nikomboe na unihurumie.

12 [d]Miguu yangu imesimama katika
uwanja tambarare;
katika kusanyiko kuu nitamsifu
BWANA.

### Zaburi 27

*Sala Ya Kusifu*

*Zaburi ya Daudi.*

1 [e]BWANA ni nuru yangu na wokovu
wangu,
nimwogope nani?
BWANA ni ngome ya uzima wangu,
nimhofu nani?
2 [f]Waovu watakaposogea dhidi yangu
ili wanile nyama yangu,
adui zangu na watesi wangu
watakaponishambulia,
watajikwaa na kuanguka.
3 [g]Hata jeshi linizunguke pande zote,
moyo wangu hautaogopa;
hata vita vitokee dhidi yangu,
hata hapo nitakuwa na ujasiri.

4 [h]Jambo moja ninamwomba BWANA,
hili ndilo ninalolitafuta:
niweze kukaa nyumbani mwa
BWANA
siku zote za maisha yangu,
niutazame uzuri wa BWANA
na kumtafuta hekaluni mwake.
5 [i]Kwa kuwa siku ya shida,
atanihifadhi salama katika
maskani yake,
atanificha uvulini mwa hema yake
na kuniweka juu kwenye
mwamba.
6 [j]Kisha kichwa changu kitainuliwa
juu ya adui zangu
wanaonizunguka.
Katika maskani yake nitatoa dhabihu
kwa kelele za shangwe;
nitamwimbia BWANA na kumsifu.

7 [k]Isikie sauti yangu nikuitapo, Ee
BWANA,
unihurumie na unijibu.
8 [l]Moyo wangu unasema kuhusu
wewe,
"Utafute uso wake!"
Uso wako, BWANA "Nitautafuta."
9 [m]Usinifiche uso wako,
usimkatae mtumishi wako kwa
hasira;
wewe umekuwa msaada wangu.
Usinikatae wala usiniache,
Ee Mungu Mwokozi wangu.
10 Hata kama baba yangu na mama
wakiniacha,
BWANA atanipokea.
11 [n]Nifundishe njia yako, Ee BWANA,
niongoze katika njia iliyonyooka
kwa sababu ya watesi wangu.

---

[a]**26:9** Za 5:6; 28:3; 55:23; 139:19; Mit 29:10
[b]**26:10** Za 21:11; Isa 1:23; Ay 36:18; Eze 22:12
[c]**26:11** Za 31:5; 69:18; 119:134; Tit 2:14
[d]**26:12** Za 22:25; 27:11; Ay 36:18; Lk 6:17; Isa 26:7; 40:3-4; 45:13; Zek 4:7
[e]**27:1** 2Sam 22:29; Ay 13:5; Za 3:8; 9:9; 56:4, 11; 118:6; Kut 15:2
[f]**27:2** Za 9:3; 20:8; 37:24; Dan 11:19; Rum 11:11
[g]**27:3** Mwa 4:7; Za 3:6; Ay 4:6
[h]**27:4** Lk 10:42; Za 23:6; 61:4
[i]**27:5** Ay 38:23; Za 12:7, 8; 40:2
[j]**27:6** 2Sam 22:49; Za 3:3; 33:2; 54:6; 18:48; 22:12; 92:1; 50:14; 107:22; 116:17; 147:7; Ezr 3:13; Ay 22:26; Kut 15:1; Efe 5:19
[k]**27:7** Za 4:1; 5:3; 18:6; 55:17; 119:149; 130:2; Isa 28:23
[l]**27:8** 1Nya 16:11
[m]**27:9** Za 2:5; 119:8; 18:46; 22:24; 37:28; Mwa 49:25; Kum 31:17; 33:29; 4:31; Isa 41:17; 62:12; Yer 14:9
[n]**27:11** Ezr 8:21; Za 5:8; 72:4; 78:42; 106:10; Yer 21:12; Kut 33:13

12 [a]Usiniachilie kwa nia za adui zangu,
kwa maana mashahidi wa uongo
wameinuka dhidi yangu,
wakipumua ujeuri.

13 [b]Nami bado nina tumaini hili:
nitauona wema wa BWANA
katika nchi ya walio hai.
14 [c]Mngojee BWANA,
uwe hodari na mwenye moyo
mkuu,
nawe, umngojee BWANA.

## Zaburi 28

*Kuomba Msaada*

*Zaburi ya Daudi.*

1 [d]Ninakuita wewe, Ee BWANA,
Mwamba wangu;
usiwe kwangu kama kiziwi.
Kwa sababu ukinyamaza
nitafanana na walioshuka shimoni.
2 [e]Sikia kilio changu unihurumie
ninapokuita kwa ajili ya msaada,
niinuapo mikono yangu kuelekea
Patakatifu pa Patakatifu pako.

3 [f]Usiniburute pamoja na waovu,
pamoja na hao watendao mabaya,
ambao huzungumza na jirani zao
maneno mazuri,
lakini mioyoni mwao wameficha
chuki.
4 [g]Walipe sawasawa na matendo yao,
sawasawa na matendo yao maovu;
walipe sawasawa na kazi za mikono
yao,
uwalipe wanavyostahili.

5 [h]Kwa kuwa hawaheshimu kazi za
BWANA,
na yale ambayo mikono yake
imetenda,
atawabomoa na kamwe
hatawajenga tena.

6 [i]BWANA asifiwe,
kwa maana amesikia kilio changu
nikimwomba anihurumie.
7 [j]BWANA ni nguvu zangu na ngao
yangu,
moyo wangu umemtumaini yeye,
nami nimesaidiwa.
Moyo wangu unarukaruka kwa
furaha
nami nitamshukuru kwa wimbo.

8 [k]BWANA ni nguvu ya watu wake,
ngome ya wokovu kwa mpakwa
mafuta wake.
9 [l]Waokoe watu wako na uubariki
urithi wako;
uwe mchungaji wao na uwabebe
milele.

## Zaburi 29

*Sauti Ya BWANA Wakati Wa Dhoruba*

*Zaburi ya Daudi.*

1 [m]Mpeni BWANA, enyi mashujaa,
mpeni BWANA utukufu na nguvu.
2 [n]Mpeni BWANA utukufu unaostahili
jina lake;
mwabuduni BWANA katika uzuri
wa utakatifu wake.

---

[a]**27:12** Kum 19:16; Mt 26:60; Mdo 6:13; 1Kor 15:15
[b]**27:13** Kut 33:19; 2Nya 6:41; Za 33:6; 31:19; 145:7; Ay 18:13
[c]**27:14** Efe 6:10; Amu 5:21; Kum 1:21; Sef 3:8; Hab 2:3; Za 33:20; 130:5, 6; Mdo 1:4; Isa 8:17; 30:18
[d]**28:1** Kum 1:45; Es 4:14; Ay 33:18
[e]**28:2** Za 17:1; 61:1; 5:7; 11:4; 116:1; 63:4; 130:2; 142:1; 143:1; 141:2; Mao 2:19; Ezr 9:5; 1Tim 2:8
[f]**28:3** Za 12:2; 26:4; 55:21; Yer 9:8
[g]**28:4** Za 62:12; 2Tim 4:14; Mao 3:64; Ufu 18:6; 22:12
[h]**28:5** Isa 5:12
[i]**28:6** Mwa 24:27; Efe 1:3; 2Kor 1:3; 1Pet 1:3
[j]**28:7** Za 144:9; 13:5; 16:9; 33:3; 40:3; 69:30; 149:1; 18:1; 112:7; Isa 26:3; Kum 16:15
[k]**28:8** Za 18:1; 27:1; 20:6; Kut 15:2; Hab 3:13
[l]**28:9** Za 78:52, 71; 80:1; 106:47; 118:25; 23:1; 1Nya 6:35; 11:2; Kut 34:9; Isa 40:11; 46:3; 63:9; Eze 34:12; Yer 31:10; Mik 7:14; Kum 1:31; 32:11
[m]**29:1** 1Nya 16:28; 2Sam 1:19; Isa 10:13; Za 103:20; 8:1
[n]**29:2** 1Nya 16:29; Za 96:7-9

3 [a]Sauti ya BWANA iko juu ya maji;
Mungu wa utukufu hupiga radi,
BWANA hupiga radi juu ya maji
makuu.

4 [b]Sauti ya BWANA ina nguvu;
sauti ya BWANA ni tukufu.
5 [c]Sauti ya BWANA huvunja mierezi;
BWANA huvunja vipande vipande
mierezi ya Lebanoni.
6 [d]Hufanya Lebanoni irukaruke kama
ndama,
Sirioni[e] urukaruke kama mwana
nyati.
7 [f]Sauti ya BWANA hupiga kwa miali
ya umeme wa radi.
8 [g]Sauti ya BWANA hutikisa jangwa;
BWANA hutikisa Jangwa la
Kadeshi.
9 [h]Sauti ya BWANA huzalisha ayala,
na huuacha msitu wazi.
Hekaluni mwake wote wasema,
"Utukufu!"

10 [i]BWANA huketi akiwa ametawazwa
juu ya gharika;
BWANA ametawazwa kuwa
Mfalme milele.
11 [j]BWANA huwapa watu wake nguvu;
BWANA huwabariki watu wake
kwa kuwapa amani.

## Zaburi 30

*Maombi Ya Shukrani*

*Utenzi wa kuweka wakfu hekalu. Zaburi ya Daudi.*

1 [k]Nitakutukuza wewe, Ee BWANA,
kwa kuwa umeniinua kutoka
vilindi,
na hukuacha adui zangu
washangilie juu yangu.
2 [l]Ee BWANA, Mungu wangu, nilikuita
unisaidie
na wewe umeniponya.
3 [m]Ee BWANA, umenitoa Kuzimu,
umeniokoa nisishuke kwenye
shimo la mauti.

4 [n]Mwimbieni BWANA, enyi watakatifu
wake;
lisifuni jina lake takatifu.
5 [o]Kwa maana hasira yake ni ya muda
mfupi,
bali upendo wake hudumu siku
zote.
Inawezekana kilio kiwepo usiku
kucha,
lakini asubuhi kukawa na furaha.

6 [p]Nilipofanikiwa nilisema,
"Sitatikiswa kamwe."
7 [q]Ee BWANA, uliponijalia,
uliuimarisha mlima wangu,
lakini ulipouficha uso wako
nilifadhaika.

8 Kwako wewe, Ee BWANA, niliita,
kwa Bwana niliomba rehema:

---

[a]**29:3** Ay 37:5; Za 24:7; 18:13; 46:6; 68:33; 77:17; Mdo 7:2; 1Sam 2:10; Yer 10:13; 25:30; Yoe 2:11; Amo 1:2; Kut 15:10
[b]**29:4** Za 68:33
[c]**29:5** Amu 9:15
[d]**29:6** Za 92:10; 114:4; Kum 3:9; Ay 39:9; Hes 23:22
[e]6 Yaani Mlima Hermoni.
[f]**29:7** Eze 1:14; Ufu 8:5
[g]**29:8** Hes 13:26; 20:1
[h]**29:9** Isa 2:13; Eze 27:6; Amo 2:9; Za 26:8
[i]**29:10** Mwa 6:17; Kut 15:18
[j]**29:11** Za 18:1; 28:8; 68:35; Law 26:6; Hes 6:26; Isa 40:29

[k]**30:1** Kut 15:2; Isa 14:15; Ay 11:8; Mit 9:18; Za 63:9; 107:26; 22:17
[l]**30:2** Za 5:2; 88:13; 6:2-4; Hes 12:13
[m]**30:3** Za 40:1, 2; 16:10; 56:13; 28:1; 55:23; 69:15; 86:13; 143:7; Mit 1:12; Isa 38:17; Yon 2:6
[n]**30:4** Za 33:1; 47:7; 68:4; 16:3; 33:21; 103:1; 145:21; Kut 3:15
[o]**30:5** Za 103:9; 126:6; 6:6; 2Sam 15:30; 2Kor 4:17; Ezr 3:1; Ay 14:13; Yer 31:6
[p]**30:6** Ay 29:18
[q]**30:7** Kum 31:17; Za 104:29

9 [a]"Kuna faida gani katika kuangamia kwangu?
Katika kushuka kwangu shimoni?
Je, mavumbi yatakusifu?
Je, yatatangaza uaminifu wako?
10 [b]Ee BWANA, unisikie na kunihurumia,
Ee BWANA, uwe msaada wangu."

11 [c]Uligeuza maombolezo yangu kuwa kucheza,
ulinivua nguo za gunia ukanivika shangwe,
12 [d]ili moyo wangu uweze kukusifu na usikae kimya.
Ee BWANA Mungu wangu, nitakushukuru milele.

## Zaburi 31

*Maombi Na Sifa Kwa Kuokolewa Kutoka Kwa Adui*

*Kwa mwimbishaji. Zaburi ya Daudi.*

1 [e]Ee BWANA, nimekukimbilia wewe,
usiache nikaaibika kamwe,
kwa haki yako uniokoe.
2 [f]Nitegee sikio lako,
uje uniokoe haraka;
uwe kwangu mwamba wa kimbilio,
ngome imara ya kuniokoa.
3 [g]Kwa kuwa wewe ni mwamba wangu na ngome yangu,
uniongoze na kunilinda kwa ajili ya jina lako.
4 [h]Uniepushe na mtego niliotegewa,
maana wewe ndiwe kimbilio langu.
5 [i]Ninaikabidhi roho yangu mikononi mwako,
unikomboe Ee BWANA, uliye Mungu wa kweli.

6 [j]Ninawachukia wale wanaong'ang'ania sanamu batili;
mimi ninamtumaini BWANA.
7 [k]Nitafurahia na kushangilia upendo wako,
kwa kuwa uliona mateso yangu
na ulijua maumivu ya nafsi yangu.
8 [l]Hukunikabidhi kwa adui yangu
bali umeiweka miguu yangu mahali penye nafasi.

9 [m]Ee BWANA unihurumie, kwa kuwa niko kwenye shida;
macho yangu yanafifia kwa huzuni,
nafsi yangu na mwili wangu kwa sikitiko.
10 [n]Maisha yangu yamedhoofika kwa majonzi,
naam, miaka yangu kwa kulia kwa maumivu makali;
nguvu zangu zinaisha kwa ajili ya mateso,
na mifupa yangu inachakaa.
11 [o]Kwa sababu ya adui zangu wote,
nimedharauliwa kabisa na jirani zangu,
hata kwa rafiki zangu nimekuwa tisho,
wale wanionao barabarani hunikimbia.
12 [p]Nimesahaulika miongoni mwao kama mtu aliyekufa,
nimekuwa kama chombo cha mfinyanzi kilichovunjika.

---

[a]**30:9** Ay 33:18; Isa 38:18; Za 6:5; 88:11; 115:17
[b]**30:10** Za 17:1; 4:1; 20:2
[c]**30:11** 2Sam 3:31; 6:14; Es 4:1; Kut 15:20; Za 35:13; 16:9; Kum 16:15
[d]**30:12** Za 35:18; 75:1; 118:21; 44:8; 52:9; Ufu 11:17
[e]**31:1** Za 7:1; 5:8
[f]**31:2** Za 6:4
[g]**31:3** Za 18:2; 23:3; Yer 14:7
[h]**31:4** 1Sam 28:9; Ay 18:10; Za 9:9
[i]**31:5** Lk 23:46; Ebr 6:18; Mdo 7:59; Isa 45:19; 65:16; 2Tim 1:12
[j]**31:6** Kum 32:21; Za 4:5
[k]**31:7** Yn 10:27; Lk 22:44; Za 25:17
[l]**31:8** Za 18:19; Kum 32:30; 2Sam 22:20
[m]**31:9** Za 4:1; 6:7; 63:1
[n]**31:10** Za 6:6; 22:5; 32:4; 38:10; 73:26; 25:18; 6:2
[o]**31:11** Kum 30:7; Za 3:7; 25:19; 102; 22:6; 38:11; 88:8
[p]**31:12** Za 28:1; 88:4

13 [a]Kwa maana nimesikia maneno
niliyosingiziwa na wengi;
vitisho viko pande zote;
kwa kuwa wamefanya mashauri
dhidi yangu,
na kula njama kuniua.

14 [b]Lakini mimi ninakutumaini wewe
peke yako, Ee BWANA;
nimesema, "Wewe ndiwe Mungu
wangu."
15 [c]Siku za maisha yangu ziko mikononi
mwako,
uniokoe mikononi mwa adui
zangu
na wale wanifuatiao.
16 [d]Mwangazie mtumishi wako uso
wako,
uniokoe kwa ajili ya upendo wako
usiokoma.
17 [e]Usiniache niaibike, Ee BWANA,
kwa maana nimekulilia wewe,
bali waovu waaibishwe
na kunyamazishwa Kuzimu.
18 [f]Midomo yao isemayo uongo na
inyamazishwe,
kwa maana kwa kiburi na dharau
wao husema kwa majivuno
dhidi ya wenye haki.

19 [g]Tazama jinsi ulivyo mkuu wema
wako,
uliowawekea akiba wakuchao,
ambao huwapa wale wakukimbiliao
machoni pa watu.
20 [h]Unawahifadhi katika uvuli wa
uwepo wako
kutokana na hila za wanadamu;
katika makao yako huwaweka
salama
kutokana na ndimi za mashtaka.

21 [i]Atukuzwe BWANA,
kwa kuwa amenionyesha upendo
wake wa ajabu
nilipokuwa katika mji
uliozingirwa.
22 [j]Katika hofu yangu nilisema,
"Nimekatiliwa mbali na macho
yako!"
Hata hivyo ulisikia kilio changu
ukanihurumia nilipokuita
unisaidie.

23 [k]Mpendeni BWANA ninyi watakatifu
wake wote!
BWANA huwahifadhi waaminifu,
lakini wenye kiburi huwalipiza
kikamilifu.
24 [l]Kuweni hodari na mjipe moyo,
ninyi nyote mnaomtumaini
BWANA.

## Zaburi 32

*Furaha Ya Msamaha*

*Zaburi ya Daudi. Funzo.*

1 [m]Heri mtu yule ambaye
amesamehewa makosa yake,
ambaye dhambi zake
zimefunikwa.
2 [n]Heri mtu yule ambaye BWANA
hamhesabii dhambi,
na ambaye rohoni mwake
hamna udanganyifu.

3 [o]Niliponyamaza, mifupa yangu
ilichakaa
kwa kulia kwa maumivu makali
mchana kutwa.

---

[a]**31:13** Law 19:16; Isa 13:8; Za 50:20; 41:7; 56:6; 71:10; 83:3; Ay 18:11; Yer 6:25; 20:3, 10; 46:5; 49:5; Mao 2:22; Mwa 37:18; Mt 12:14; 27:1
[b]**31:14** Za 4:5
[c]**31:15** Ay 14:5
[d]**31:16** Hes 6:25; Dan 9:17; Za 4:6; 6:4
[e]**31:17** Za 22:5; 94:17; 115:17; 25:2; 1Sam 2:9
[f]**31:18** Za 120:2; 12:3; Mit 10:18; 26:24; 1Sam 2:3; Yud 15
[g]**31:19** Za 27:13; 23:5; Isa 64:4; 1Kor 2:9; Rum 11:22
[h]**31:20** Za 55:8; 27:5; 17:8; Mwa 37:18; Ay 5:21
[i]**31:21** Za 28:6; 17:7; 1Sam 23:7
[j]**31:22** Za 116:11; 37:9; 88:5; 6:9; 66:19; 116:1; 145:19; Ay 6:9; 17:1; Isa 38:12
[k]**31:23** Za 4:3; 94:2; 18:25; Ufu 2:10; Kum 32:41; 1Pet 1:5
[l]**31:24** Za 27:14
[m]**32:1** Za 85:2; 103:3; Rum 4:6
[n]**32:2** Rum 4:7-8; 5:13; Yn 1:47; Ufu 14:5; 2Kor 1:12; Law 17:4
[o]**32:3** Ay 31:34; 31:10; 3:24; Za 6:6

4 [a]Usiku na mchana
mkono wako ulinilemea,
nguvu zangu zilinyonywa
kama vile katika joto la kiangazi.
5 [b]Kisha nilikujulisha dhambi yangu
wala sikuficha uovu wangu.
Nilisema, “Nitaungama
makosa yangu kwa BWANA.”
Ndipo uliponisamehe
hatia ya dhambi yangu.

6 [c]Kwa hiyo kila mtu mcha Mungu
akuombe
wakati unapopatikana,
hakika maji makuu yatakapofurika
hayatamfikia yeye.
7 [d]Wewe ndiwe mahali pangu pa
kujificha,
utaniepusha na taabu
na kunizunguka kwa nyimbo za
wokovu.

8 [e]Nitakufundisha na kukuonyesha
njia utakayoiendea;
nitakushauri na kukuangalia.
9 [f]Usiwe kama farasi au nyumbu
wasio na akili,
ambao ni lazima waongozwe kwa
lijamu na hatamu
la sivyo hawatakukaribia.
10 [g]Mtu mwovu ana taabu nyingi,
bali upendo usio na kikomo wa
BWANA
unamzunguka mtu
anayemtumaini.

11 [h]Shangilieni katika BWANA na
mfurahi, enyi wenye haki!
Imbeni, nyote mlio wanyofu wa
moyo!

## Zaburi 33

*Ukuu Na Wema Wa Mungu*

1 [i]Mwimbieni BWANA kwa furaha,
enyi wenye haki;
kusifu kunawapasa wanyofu wa
moyo.
2 [j]Msifuni BWANA kwa kinubi,
mwimbieni sifa kwa zeze la nyuzi
kumi.
3 [k]Mwimbieni wimbo mpya;
pigeni kwa ustadi, na mpaze sauti
za shangwe.

4 [l]Maana neno la BWANA ni haki na
kweli,
ni mwaminifu kwa yote atendayo.
5 [m]BWANA hupenda uadilifu na haki;
dunia imejaa upendo wake
usiokoma.

6 [n]Kwa neno la BWANA mbingu
ziliumbwa,
jeshi lao la angani kwa pumzi ya
kinywa chake.
7 [o]Ameyakusanya maji ya bahari
kama kwenye chungu;
vilindi vya bahari
ameviweka katika ghala.
8 [p]Dunia yote na imwogope BWANA,
watu wote wa dunia wamche.

---

[a]**32:4** 1Sam 5:6; Ay 9:34; Za 38:2; 39:10; 22:15
[b]**32:5** Ay 31:33; Mit 28:13; Lk 15:18; Za 103:12; Law 26:40; Yn 1:9
[c]**32:6** Za 69:13; Yn 7:34; Isa 55:6; Za 69:1; 43:2; Kut 15:10; 1Tim 1:16
[d]**32:7** Za 9:9; Amu 9:35; 5:1; Mit 18:10; Isa 4:6; Mt 23:37; Kol 3:3
[e]**32:8** Za 25:8; 34:11; 33:18; Isa 48:17
[f]**32:9** Ay 30:11; 39:10; Yak 3:3
[g]**32:10** Rum 2:9; Za 4:5; Mit 16:20; Yer 17:7; Mit 13:21; 16:20
[h]**32:11** Za 64:10
[i]**33:1** Za 64:10; 101:1; 147:1; 11:7
[j]**33:2** Mwa 4:21; 1Kor 14:7; Ufu 5:8; Za 92:3; 144:9
[k]**33:3** Za 40:3; 35:27; 47:1; Isa 42:10; Ufu 5:9; Ay 3:7
[l]**33:4** Ufu 19:9; 22:6; Za 19:8; 18:25; 119:142; 25:10
[m]**33:5** Za 11:7; 6:4
[n]**33:6** Ebr 11:3; Kut 8:19; Mwa 1:3, 16; 2Nya 2:12; Yn 1:1-3; Ay 26:13
[o]**33:7** Mwa 1:10; Yos 3:16
[p]**33:8** Kum 6:13; 14:23; Za 2:11; 49:1; Isa 18:3; Mik 1:2

9 [a]Kwa maana Mungu alisema, na ikawa,
aliamuru na ikasimama imara.
10 [b]BWANA huzuia mipango ya mataifa,
hupinga makusudi ya mataifa.
11 [c]Lakini mipango ya BWANA inasimama imara milele,
makusudi ya moyo wake kwa vizazi vyote.

12 [d]Heri taifa ambalo BWANA ni Mungu wao,
watu ambao aliwachagua kuwa urithi wake.
13 [e]Kutoka mbinguni BWANA hutazama chini
na kuwaona wanadamu wote;
14 [f]kutoka maskani mwake huwaangalia
wote wakaao duniani:
15 [g]yeye ambaye huumba mioyo yao wote,
ambaye huangalia kila kitu wanachokitenda.
16 [h]Hakuna mfalme aokokaye kwa ukubwa wa jeshi lake;
hakuna shujaa aokokaye kwa wingi wa nguvu zake.
17 [i]Farasi ni tumaini la bure kwa wokovu,
licha ya nguvu zake nyingi, hawezi kuokoa.
18 [j]Lakini macho ya BWANA yako kwa wale wamchao,
kwa wale tumaini lao liko katika upendo wake usio na kikomo,
19 [k]ili awaokoe na mauti,
na kuwahifadhi wakati wa njaa.

20 [l]Sisi tunamngojea BWANA kwa matumaini,
yeye ni msaada wetu na ngao yetu.
21 [m]Mioyo yetu humshangilia,
kwa maana tunalitumainia jina lake takatifu.
22 [n]Upendo wako usio na mwisho ukae juu yetu, Ee BWANA,
tunapoliweka tumaini letu kwako.

## Zaburi 34[o]

*Sifa Na Wema Wa Mungu*

*Zaburi ya Daudi, alipojifanya mwendawazimu mbele ya Abimeleki, ambaye alimfukuza, naye akaondoka.*

1 [p]Nitamtukuza BWANA nyakati zote,
sifa zake zitakuwa midomoni mwangu siku zote.
2 [q]Nafsi yangu itajisifu katika BWANA,
walioonewa watasikia na wafurahi.
3 [r]Mtukuzeni BWANA pamoja nami,
naam, na tulitukuze jina lake pamoja.

4 [s]Nilimtafuta BWANA naye akanijibu,
akaniokoa kwenye hofu zangu zote.
5 [t]Wale wamtazamao hutiwa nuru,
nyuso zao hazifunikwi na aibu kamwe.

---

[a]**33:9** Za 148:5; Mwa 1:3
[b]**33:10** Isa 44:25; Za 2:1; Ay 5:12
[c]**33:11** Hes 23:19; Yer 51:12, 29; Ay 23:13; Mit 19:21; Eze 38:10; Mdo 4:27, 28
[d]**33:12** Za 144:15; 65:4; 4:3; 84:4; Kum 7:6; Kut 8:22; 34:9
[e]**33:13** Za 53:2; 102:19; 11:4; 14:2; Ebr 4:13; 2Nya 16:9; Ay 28:24
[f]**33:14** Law 15:31; 1Fal 8:39
[g]**33:15** Ay 10:8; 11:11; 10:4; Yer 32:19; Isa 64:8; Hes 7:2; Za 44:21; 119:73; Mit 24:12
[h]**33:16** 1Sam 14:6
[i]**33:17** Za 20:7
[j]**33:18** Kut 3:16; Ay 36:7; Za 11:4; 6:4; 34:15; 1Pet 3:12
[k]**33:19** Za 56:13; Ay 5:20; Mdo 12:11
[l]**33:20** Za 27:14
[m]**33:21** 1Sam 2:1; Yoe 2:23; Za 30:4; 99:3
[n]**33:22** Za 6:4
[o]Zaburi hii imetungwa kila mstari ukianzia na herufi ya alfabeti ya Kiebrania zikifuatana tangu Aleph (A) hadi Taw (T); zote ni 22.
[p]**34:1** Za 71:6; Efe 5:20; 1The 5:18
[q]**34:2** Za 44:8; 69:32; 107:42; 119:74; Yer 9:24; 1Kor 1:31
[r]**34:3** Za 63:3; 86:12; Dan 4:37; Kut 15:2; Yn 17:1; Rum 15:6
[s]**34:4** Za 18:6; 77:2; 18:43; 22:4; 56:13; 86:13; Kut 32:11; Yon 2:2; Mt 7:7; Lk 11:9
[t]**34:5** Kut 34:29; Za 25:3; 44:15; 69:7; 83:16

6 [a]Maskini huyu alimwita BWANA,
naye akamsikia,
akamwokoa katika taabu zake
zote.
7 [b]Malaika wa BWANA hufanya kituo
akiwazunguka wale wamchao,
naye huwaokoa.

8 [c]Onjeni mwone kwamba BWANA ni
mwema,
heri mtu yule anayemkimbilia.
9 [d]Mcheni BWANA enyi watakatifu
wake,
kwa maana wale wamchao
hawapungukiwi na chochote.
10 [e]Wana simba wenye nguvu
hutindikiwa na kuona njaa,
bali wale wamtafutao BWANA
hawatakosa kitu chochote kilicho
chema.

11 [f]Njooni, watoto wangu, mnisikilize,
nitawafundisha kumcha BWANA.
12 [g]Yeyote kati yenu anayependa uzima
na kutamani kuziona siku nyingi
njema,
13 [h]basi auzuie ulimi wake na mabaya,
na midomo yake kutokana na
kusema uongo.
14 [i]Aache uovu, atende mema,
aitafute amani na kuifuatilia.

15 [j]Macho ya BWANA huwaelekea
wenye haki,
na masikio yake yako makini
kusikiliza kilio chao.
16 [k]Uso wa BWANA uko kinyume na
watendao maovu,
ili kufuta kumbukumbu lao
duniani.

17 [l]Wenye haki hulia, naye BWANA
huwasikia,
huwaokoa katika taabu zao zote.
18 [m]BWANA yu karibu na waliovunjika
moyo,
na huwaokoa waliopondeka roho.

19 [n]Mwenye haki ana mateso mengi,
lakini BWANA humwokoa nayo
yote,
20 [o]huhifadhi mifupa yake yote,
hata mmoja hautavunjika.

21 [p]Ubaya utamuua mtu mwovu,
nao adui za mwenye haki
watahukumiwa.
22 [q]BWANA huwakomboa watumishi
wake,
yeyote anayemkimbilia yeye
hatahukumiwa kamwe.

## Zaburi 35

*Kuomba Msaada: Kuokolewa Kutokana Na Maadui*

*Zaburi ya Daudi.*

1 [r]Ee BWANA, pingana na wale
wanaopingana nami,
upigane na hao wanaopigana
nami.
2 [s]Chukua ngao na kigao.
Inuka unisaidie.

---

[a]**34:6** Za 25:17; 2Sam 22:1
[b]**34:7** Mwa 32:1; Ebr 1:14; Dan 3:28; 6:22; Mt 18:10; Isa 31:5; Za 22:4; 37:40; 41:1; 97:10; Mdo 12:11; 2Fal 16:17
[c]**34:8** Ebr 6:5; 1Pet 2:3; Za 2:12
[d]**34:9** Flp 4:19; Za 23:1; Kum 6:13; Ufu 14:7
[e]**34:10** Za 23:1
[f]**34:11** Za 66:16; 32:8; 19:9
[g]**34:12** Mhu 3:13; 1Pet 3:10
[h]**34:13** 1Pet 2:22; Za 39:1; 141:3; Mit 13:3; 21:23; Yak 1:26; Za 12:2
[i]**34:14** Za 37:27; Isa 1:17; 3Yn 11; Rum 14:19
[j]**34:15** Ay 36:7; 23:10; Mal 3:16; Yn 9:31; Za 33:18
[k]**34:16** Law 17:10; Za 9:6; Yer 23:30; 44:11; Mit 10:7; Kut 17:14; 1Pet 3:10-12
[l]**34:17** Za 145:19
[m]**34:18** Kum 4:7; Za 51:17; 119:151; 145:18; 109:16; 147:3; Isa 50:8; 61:1
[n]**34:19** Za 34:17; 25:17; Ay 5:19; 2Tim 3:11
[o]**34:20** Yn 19:34
[p]**34:21** Za 7:9; 9:16; 37:20; 73:27; 94:23; 106:43; 112:10; 140:11; Mit 14:32; 24:16
[q]**34:22** Kut 6:6; 15:13; Lk 1:68; Ufu 14:3; Za 2:12; 103:4; 2Sam 4:9
[r]**35:1** 1Sam 24:15; Kut 14:14
[s]**35:2** Za 3:3, 7; Ay 17:3; Mwa 50:24; 35:3; Hes 25:7; Za 27:1; Yos 8:18

3 Inua mkuki wako na fumo[a] lako
dhidi ya hao wanaonifuatia.
Iambie nafsi yangu,
"Mimi ni wokovu wako."

4 [b]Wafedheheshwe na waaibishwe
wale wanaotafuta uhai wangu.
Wanaofanya shauri kuniangamiza
warudishwe nyuma kwa hofu.
5 [c]Wawe kama makapi
yapeperushwayo na upepo,
malaika wa BWANA akiwafukuza.
6 Njia yao na iwe giza na ya utelezi,
malaika wa BWANA akiwafuatilia.
7 [d]Kwa vile walinifichia wavu wao
bila sababu,
na bila sababu wamenichimbia
shimo,
8 [e]maafa na yawapate ghafula:
wavu walionifichia na uwatege
wenyewe,
na waanguke katika shimo hilo,
kwa maangamizo yao.
9 [f]Ndipo nafsi yangu itashangilia
katika BWANA
na kuufurahia wokovu wake.
10 [g]Nitapaza sauti yangu nikisema,
"Ni nani aliye kama wewe, Ee
BWANA?
Wewe huwaokoa maskini kutokana
na wale walio na nguvu
kuliko wao,
maskini na mhitaji kutokana na
wanaowanyang'anya!"

11 [h]Mashahidi wakatili wanainuka,
wananiuliza mambo nisiyoyajua.
12 [i]Wananilipa baya kwa jema
na kuiacha nafsi yangu ukiwa.
13 [j]Lakini walipokuwa wagonjwa,
nilivaa nguo ya gunia
na nikajinyenyekesha kwa
kufunga.
Maombi yangu yaliponirudia bila
kujibiwa,
14 [k]niliendelea kuomboleza
kama vile wao ni rafiki au ndugu.
Niliinamisha kichwa chini kwa
huzuni
kama ninayemwombolezea mama
yangu.
15 [l]Lakini nilipojikwaa,
walikusanyika kwa shangwe;
washambuliaji walijikusanya dhidi
yangu
bila mimi kujua.
Walinisingizia pasipo kukoma.
16 [m]Kama watu wasiomcha Mungu,
wamenidhihaki,
wamenisagia meno.
17 [n]Ee BWANA, utatazama mpaka lini?
Niokoe maisha yangu na
maangamizi yao,
uhai wangu wa thamani
kutokana na simba hawa.
18 [o]Nami nitakushukuru mbele ya
kusanyiko kubwa,
nitakusifu katikati ya watu wengi.

19 [p]Usiwaache wale wanaonisimanga,
wale ambao ni adui zangu bila
sababu;
usiwaache wale ambao ni adui zangu
bila sababu
wakonyeze jicho kwa hila.

---

[a]3 Fumo ni sawa na sagai, maana yake ni mkuki mfupi.
[b]**35:4** Za 38:12; 40:14; 69:6, 19; 70:2; 83:17; 25:3; 129:5; Yer 4:30; Mal 2:9; Isa 45:16
[c]**35:5** Ay 13:25; Za 1:4; 34:7
[d]**35:7** Ay 18:8; 9:31; Za 7:4; 7:15; 55:23
[e]**35:8** Isa 47:11; 1The 5:3; Za 7:15; Mit 5:22
[f]**35:9** Za 2:11; 9:14; 13:5; 27:1; Lk 1:47; 1Sam 2:1; Isa 61:10; Ebr 3:18
[g]**35:10** Kut 9:14; Za 12:5; 71:19; 18:17, 31; 113:5; 37:14; 86:1; 74:21; 109:16; 140:12; Isa 41:17
[h]**35:11** Kut 23:1; Mt 26:60
[i]**35:12** Yer 18:20; Za 38:20; 109:5; Mit 17:13
[j]**35:13** 2Sam 3:31; 1Fal 20:31; Za 30:11; 69:10, 11; 109:24; Ay 30:25
[k]**35:14** Za 38:6; 42:9; 43:2
[l]**35:15** Ay 31:29; 16:10
[m]**35:16** Za 22:7; Mk 10:34; 9:18; Ay 16:9; Mdo 7:54
[n]**35:17** Za 6:3; 22:20, 21; 57:4; 58:6
[o]**35:18** Za 22:20, 25; 42:4; 109:30
[p]**35:19** Za 9:13; 38:19; 69:4; Yn 15:25; Mit 6:13; 10:10

[20] [a]Hawazungumzi kwa amani,
bali wanatunga mashtaka ya uongo
dhidi ya wale wanaoishi
kwa utulivu katika nchi.
[21] [b]Hunifumbulia vinywa vyao wakisema, “Aha! Aha!
Kwa macho yetu wenyewe tumeliona.”

[22] [c]Ee BWANA, umeona hili, usiwe kimya.
Usiwe mbali nami, Ee BWANA.
[23] [d]Amka, inuka unitetee!
Unipiganie Mungu wangu na Bwana wangu.
[24] [e]Nihukumu kwa haki yako, Ee BWANA Mungu wangu,
sawasawa na haki yako;
usiwaache wakusimange.
[25] [f]Usiwaache wafikiri, “Aha, hili ndilo tulilotaka!”
Au waseme, “Tumemmeza.”

[26] [g]Wote wanaofurahia dhiki yangu
waaibishwe na wachanganyikiwe;
hao wanaojiinua dhidi yangu
wavikwe aibu na dharau.
[27] [h]Wale wanaofurahia hukumu yangu ya haki
wapige kelele za shangwe na furaha;
hebu waseme siku zote, “BWANA atukuzwe,
ambaye amefurahia mafanikio ya mtumishi wake.”
[28] [i]Ulimi wangu utanena haki yako
na sifa zako mchana kutwa.

## Zaburi 36

*Uovu Wa Mwanadamu*

*Kwa mwimbishaji. Zaburi ya Daudi mtumishi wa BWANA.*

[1] [j]Kuna neno moyoni mwangu
kuhusu hali ya dhambi ya mwovu.
Hakuna hofu ya Mungu
mbele ya macho yake.
[2] [k]Kwa kuwa machoni pake mwenyewe hujisifu mno
hata hawezi kugundua au kuichukia dhambi yake.
[3] [l]Maneno ya kinywa chake ni maovu na ya udanganyifu,
ameacha kuwa mwenye hekima na kutenda mema.
[4] [m]Hata kitandani mwake hupanga hila mbaya,
hujitia katika njia ya dhambi
na hakatai lililo baya.

[5] [n]Upendo wako, Ee BWANA, unafika hadi mbinguni,
uaminifu wako hadi kwenye anga.
[6] [o]Haki yako ni kama milima mikubwa,
hukumu zako ni kama kilindi kikuu.
Ee BWANA, wewe huwahifadhi
mwanadamu na mnyama.
[7] [p]Upendo wako usiokoma
ni wa thamani mno!
Watu wakuu na wadogo
hujificha uvulini wa mbawa zako.

---

[a]**35:20** Za 38:12; 55:21; Yer 9:8; Mik 6:12
[b]**35:21** Ay 16:10; Eze 25:3; Za 40:15; 70:3
[c]**35:22** Kut 3:7; Za 10:1, 14
[d]**35:23** Za 7:6; 80:2; 17:13; 1Sam 24:15
[e]**35:24** Za 22:17; 7:8; 26:11; 2The 1:6
[f]**35:25** Mit 1:12; Za 35:21; 124:3; Mao 2:16
[g]**35:26** Za 22:17; 4:1; 109:29; 38:16; Ay 8:22; 19:5; Mik 7:10
[h]**35:27** Za 9:4; 20:5; 33:3; 147:11; 149:4; Ay 17:3
[i]**35:28** Za 5:8; 51:14; 71:15, 24; 72:15
[j]**36:1** Ay 21:16; 23:15; Yer 2:19; 36:16, 24; Rum 3:18; Mit 8:13; Mwa 20:11; Mhu 12:3
[k]**36:2** Kum 29:19
[l]**36:3** Yer 4:22; 13:23; Za 10:7; 5:6, 9; 43:1; 144:8, 11; 94:8; Ay 5:13; Isa 44:20; Amo 3:10
[m]**36:4** Mik 2:1; Rum 12:9; Isa 65:2; Za 52:3
[n]**36:5** Za 89:1; 119:90; 108:4; 57:10; 89:2; 71:19; 103:11
[o]**36:6** Za 5:8; 68:15; Mwa 1:2; Za 104:14; 7:11; 145:9; Neh 9:6; Rum 11:33; Ay 7:20; 11:8
[p]**36:7** Za 6:4; 17:8; 57:1; 91:4; Rut 2:12

8 [a]Wanajifurahisha katika wingi
nyumbani mwako,
nawe utawanywesha katika mto
wa furaha zako.
9 [b]Kuwa pamoja nawe ni kijito cha
uzima,
katika nuru yako twaona nuru.

10 [c]Dumisha upendo wako kwa wale
wanaokujua wewe,
haki yako kwa wale walio
wanyofu wa moyo.
11 [d]Mguu wa mwenye kiburi usije dhidi
yangu,
wala mkono wa mwovu
usinifukuze.
12 [e]Angalia jinsi watenda mabaya
walivyoanguka:
wametupwa chini, hawawezi
kuinuka!

## Zaburi 37[f]

*Mwisho Wa Mwovu Na Urithi Wa Mwenye Haki*

*Zaburi ya Daudi.*

1 [g]Usisumbuke kwa ajili ya watendao
maovu,
wala usiwaonee wivu watendao
mabaya,
2 [h]kwa maana kama majani
watanyauka mara,
kama mimea ya kijani watakufa
mara.
3 [i]Mtumaini Bwana na utende yaliyo
mema;
Kaa katika nchi ukafurahie
malisho salama.
4 [j]Jifurahishe katika Bwana
naye atakupa haja za moyo wako.

5 [k]Mkabidhi Bwana njia yako,
mtumaini yeye, naye atatenda hili:
6 [l]Yeye atafanya haki yako ing'ae
kama mapambazuko,
na hukumu ya shauri lako kama
jua la adhuhuri.

7 [m]Tulia mbele za Bwana
na umngojee kwa uvumilivu;
usisumbuke watu wanapofanikiwa
katika njia zao,
wanapotekeleza mipango yao
miovu.

8 [n]Epuka hasira na uache ghadhabu,
usihangaike: itakuongoza tu
kutenda uovu.
9 [o]Kwa maana waovu watakatiliwa
mbali,
bali wale wanaomtumaini Bwana
watairithi nchi.

10 [p]Bado kitambo kidogo, nao waovu
hawataonekana,
ingawa utawatafuta,
hawataonekana.
11 [q]Bali wanyenyekevu watairithi nchi
na wafurahie amani tele.

---

[a]**36:8** Za 65:4; 23:2; 63:5; Yer 31:12, 14; Ufu 22:1; Isa 25:6; Ay 20:17
[b]**36:9** Isa 12:3; 2:5; 9:2; 60:1, 19; Yer 2:13; Zek 13:1; Yn 1:4; 4:10, 14; Ufu 21:6; Mdo 26:18; Efe 5:8; Kol 1:13; 1Pet 2:9; Mit 10:11; 16:22; Za 87:7; 4:6; 27:1; 76:4; 104:2
[c]**36:10** Yer 31:3; 9:24; 22:16; Za 7:10; 11:2; 94:15; 125:4
[d]**36:11** Za 71:4; 140:4
[e]**36:12** Za 18:38
[f]Zaburi hii imetungwa kila beti likianzia na herufi ya alfabeti ya Kiebrania zikifuatana tangu Aleph (A) hadi Taw (T); zote ni 22.
[g]**37:1** Mit 3:31; 3:17, 18; 24:19
[h]**37:2** 2Fal 19:26; Ay 14:2; Za 92:7; 102:4; 90:6; Yak 1:10; Isa 40:7; Za 37:38
[i]**37:3** Kum 30:20; Yn 10:9; Eze 34:14
[j]**37:4** Ay 27:10; 7:6; Wim 2:3; Za 21:2; 145:19; Mit 6:33; Isa 58:14; 1Pet 1:8
[k]**37:5** Za 4:5; 57:10; Mt 6:25; 1Pet 5:7
[l]**37:6** Ay 11:8; 7:20; 11:17; Rum 11:33; Za 145:9; 18:24; 103:17; 112:3; Mik 7:9
[m]**37:7** Kut 14:14; Yer 12:1; Isa 41:1; 38:13; Za 119:150; 40:1; 27:14; 21:11; 26:10; 130:5; Hab 3:16; Rum 8:25
[n]**37:8** Efe 4:26, 31; Ay 5:2; Kol 3:8; Mit 14:29; Za 73:3; Yak 1:19
[o]**37:9** Za 31:22; 101:8; 25:13; Mit 2:22; Isa 57:13; 40:31; 51:5, 22; 49:8, 23; 25:9; 26:8; Mt 5:5
[p]**37:10** Ay 7:10; Eze 27:30
[q]**37:11** Hes 6:26; 14:24; Mt 5:5; Law 26:6

12 [a]Waovu hula njama dhidi ya wenye haki
na kuwasagia meno,
13 [b]bali Bwana huwacheka waovu,
kwa sababu anajua siku yao inakuja.

14 [c]Waovu huchomoa upanga
na kupinda upinde,
ili wawaangushe maskini na wahitaji,
kuwachinja wale ambao njia zao ni nyofu.
15 [d]Lakini panga zao zitachoma mioyo yao wenyewe,
na pinde zao zitavunjwa.

16 [e]Bora kidogo walicho nacho wenye haki
kuliko wingi wa mali wa waovu wengi;
17 [f]kwa maana nguvu za waovu zitavunjwa,
lakini Bwana humtegemeza mwenye haki.

18 [g]Bwana anazifahamu siku za wanyofu,
na urithi wao utadumu milele.
19 [h]Siku za maafa hawatanyauka,
siku za njaa watafurahia wingi wa vitu.

20 [i]Lakini waovu wataangamia:
Adui za Bwana watakuwa
kama uzuri wa mashamba,
watatoweka,
watatoweka kama moshi.

21 [j]Waovu hukopa na hawalipi,
bali wenye haki hutoa kwa ukarimu.
22 [k]Wale wanaobarikiwa na Bwana watairithi nchi,
bali wale anaowalaani watakatiliwa mbali.

23 [l]Kama Bwana akipendezwa na njia ya mtu,
yeye huimarisha hatua zake,
24 [m]ajapojikwaa, hataanguka,
kwa maana Bwana
humtegemeza kwa mkono wake.

25 [n]Nilikuwa kijana na sasa ni mzee,
lakini sijaona kamwe wenye haki wameachwa
au watoto wao wakiombaomba chakula.
26 [o]Wakati wote ni wakarimu na hukopesha bila masharti.
Watoto wao watabarikiwa.

27 [p]Acha ubaya na utende wema,
nawe utaishi katika nchi milele.
28 [q]Kwa kuwa Bwana huwapenda wenye haki
naye hatawaacha waaminifu wake.

Watalindwa milele,
lakini uzao wa waovu utakatiliwa mbali.
29 [r]Wenye haki watairithi nchi,
na kuishi humo milele.

30 [s]Kinywa cha mwenye haki hutamka hekima,
nao ulimi wake huzungumza lililo haki.

---

[a]**37:12** Ay 16:9; Za 2:1; 31:13; 35:16; 112:10
[b]**37:13** 1Sam 26:10; Za 11:2; 35:10; 22:20; Eze 12:23
[c]**37:14** Za 22:20; 11:2; 35:10
[d]**37:15** 1Sam 2:4; Yer 49:35; Za 9:16; 46:9
[e]**37:16** Mit 15:16; 16:8; 1Tim 6:6
[f]**37:17** Za 10:15; 41:12; 140:12; 145:14; 146:7; Ay 38:15
[g]**37:18** Ay 23:10; Za 44:21; 37:27, 29
[h]**37:19** Ay 5:20
[i]**37:20** Za 34:21; 68:2; 102:3; Isa 51:6
[j]**37:21** Law 25:35; Za 112:5
[k]**37:22** Ay 5:3; Mit 3:33
[l]**37:23** Za 66:9; 121:3; 7:9; 147:11; Mit 16:9; Hes 14:8; Ay 11:15
[m]**37:24** Za 13:4; 55:22; 119:165; 145:14; 38:17; 41:12; 27:2; Mit 3:23; 10:9; 2Nya 9:8
[n]**37:25** Mwa 15:1; Za 111:5; 145:15; Ebr 13:5; Mk 10:46
[o]**37:26** Law 25:35; Kum 28:4; Za 112:2
[p]**37:27** Za 34:14; Yn 1:11; Hes 24:21
[q]**37:28** Za 11:7; 18:25; 97:10; Mwa 17:14; Kum 7:6; 32:26; Mit 2:22
[r]**37:29** Mit 2:21; Isa 34:17
[s]**37:30** Za 49:3; Mit 10:13

31 [a]Sheria ya Mungu wake imo moyoni mwake;
nyayo zake hazitelezi.

32 [b]Watu waovu huvizia wenye haki,
wakitafuta kuwaua;
33 [c]lakini BWANA hatawaacha mikononi mwao
wala hatawaacha wahukumiwe
kuwa wakosa wanaposhtakiwa.

34 [d]Mngojee BWANA,
na uishike njia yake.
Naye atakutukuza uirithi nchi,
waovu watakapokatiliwa mbali,
utaliona hilo.

35 [e]Nimemwona mtu mwovu na mkatili akistawi
kama mwerezi wa Lebanoni,
36 [f]lakini alitoweka mara na hakuonekana,
ingawa nilimtafuta, hakupatikana.

37 [g]Watafakari watu wasio na hatia,
wachunguze watu wakamilifu,
kuna mafanikio kwa mtu apendaye amani.
38 [h]Lakini watenda dhambi wote wataangamizwa,
mafanikio yao yatakatiliwa mbali.

39 [i]Wokovu wa wenye haki hutoka kwa BWANA,
yeye ni ngome yao wakati wa shida.
40 [j]BWANA huwasaidia na kuwaokoa,
huwaokoa kutoka kwa waovu na kuwahifadhi,
kwa maana wanamkimbilia.

## Zaburi 38

*Maombi Ya Mtu Anayeteseka*

*Zaburi ya Daudi. Maombi.*

1 [k]Ee BWANA, usinikemee katika hasira yako,
wala kuniadhibu katika ghadhabu yako.
2 [l]Kwa kuwa mishale yako imenichoma,
na mkono wako umenishukia.
3 [m]Hakuna afya mwilini mwangu
kwa sababu ya ghadhabu yako,
mifupa yangu haina uzima
kwa sababu ya dhambi zangu.
4 [n]Maovu yangu yamenifunika
kama mzigo usiochukulika.

5 [o]Majeraha yangu yameoza na yananuka,
kwa sababu ya upumbavu wa dhambi zangu.
6 [p]Nimeinamishwa chini na kushushwa sana,
mchana kutwa nazunguka nikiomboleza.
7 [q]Viuno vyangu vimejaa maumivu yaunguzayo,
hakuna afya mwilini mwangu.
8 [r]Nimedhoofika na kupondwa kabisa,
nasononeka kwa maumivu makuu ya moyoni.

---

[a]**37:31** Kum 6:6; 32:35; Ay 22:22
[b]**37:32** Za 10:8; 11:5
[c]**37:33** Ay 32:3; 2Pet 2:9; Za 109:31; 34:22; 79:11; 2:9
[d]**37:34** Za 27:14; 18:21; 52:6
[e]**37:35** Ay 5:3
[f]**37:36** Za 37:10; Dan 11:19; Mit 12:7; Isa 41:12
[g]**37:37** Mwa 6:9; Za 11:7; 18:25; Isa 57:1-2
[h]**37:38** Za 1:1, 2; 73:9, 19; Ay 1:1; 1The 4:17; Lk 2:25-30; Mdo 7:59, 60; 2Pet 1:14; Isa 32:17; 2Tim 4:6-8
[i]**37:39** Isa 12:2; Yon 2:8; Za 3:8; 9:9
[j]**37:40** 1Nya 5:20; Dan 3:17; Za 20:2; 18:48; 2:12; 34:7
[k]**38:1** Za 6:1
[l]**38:2** Ay 6:4
[m]**38:3** Mit 3:8; 4:22; Ay 33:19
[n]**38:4** Za 40:12; 65:3; Hes 11:14; Ezr 9:6; Lk 11:46
[o]**38:5** Za 147:3; Ay 19:17; Za 69:5; Mit 5:23; 12:23; 13:16; Mhu 10:3
[p]**38:6** Za 57:6; 145:14; 146:8; 35:14
[q]**38:7** Ay 14:22; 7:5
[r]**38:8** Za 6:3, 6; 22:1; 34:18; Mit 17:22; 5:11

9 [a]Ee BWANA, yote ninayoyaonea
shauku
yako wazi mbele zako,
kutamani kwangu sana
hakufichiki mbele zako.
10 [b]Moyo wangu unapigapiga,
nguvu zangu zimeniishia;
hata macho yangu yametiwa giza.
11 [c]Rafiki na wenzangu wananikwepa
kwa sababu ya majeraha yangu;
majirani zangu wanakaa mbali
nami.
12 [d]Wale wanaotafuta uhai wangu
wanatega mitego yao,
wale ambao wangetaka kunidhuru
huongea juu ya maangamizi
yangu;
hufanya shauri la hila mchana
kutwa.

13 [e]Mimi ni kama mtu kiziwi, asiyeweza
kusikia,
ni kama bubu, asiyeweza
kufungua kinywa chake,
14 nimekuwa kama mtu asiyesikia,
ambaye kinywa chake hakiwezi
kutoa jibu.
15 [f]Ee BWANA, ninakungojea wewe,
Ee Bwana Mungu wangu, utajibu.
16 [g]Kwa kuwa nilisema, "Usiwaache
wafurahie,
wala wasijitukuze juu yangu
mguu wangu unapoteleza."

17 [h]Kwa maana ninakaribia kuanguka,
na maumivu yangu yananiandama
siku zote.
18 [i]Naungama uovu wangu,
ninataabishwa na dhambi yangu.
19 [j]Wengi ni wale ambao ni adui zangu
hodari,
wale wanaonichukia bila sababu
ni wengi.
20 [k]Wanaolipa maovu kwa wema
wangu
hunisingizia ninapofuata lililo
jema.

21 [l]Ee BWANA, usiniache,
usiwe mbali nami, Ee Mungu
wangu.
22 [m]Ee Bwana Mwokozi wangu,
uje upesi kunisaidia.

## Zaburi 39

*Maombi Ya Mtu Anayeteseka*

*Kwa mwimbishaji. Mtindo wa Yeduthuni. Zaburi ya Daudi.*

1 [n]Nilisema, "Nitaziangalia njia zangu
na kuuzuia ulimi wangu usije
ukatenda dhambi;
nitaweka lijamu kinywani mwangu
wakati wote waovu wanapokuwa
karibu nami."
2 [o]Lakini niliponyamaza kimya na
kutulia,
hata pasipo kusema lolote jema,
uchungu wangu uliongezeka.
3 [p]Moyo wangu ulipata moto ndani
yangu,
nilipotafakari, moto uliwaka,
ndipo nikasema kwa ulimi wangu:

4 [q]"Ee BWANA, nijulishe mwisho wa
maisha yangu
na hesabu ya siku zangu;

[a]**38:9** Za 119:20; 143:7; Ay 3:24
[b]**38:10** Ay 37:1; Za 6:7; 31:10; 19:8; 88:9
[c]**38:11** Za 38:5; Lk 10:31
[d]**38:12** Za 35:4, 20; 140:5; 31:4; 141:9; 41:5
[e]**38:13** Za 115:6; 135:17; Isa 43:8; Mk 7:37
[f]**38:15** Za 27:14; 17:6; Yer 14:8
[g]**38:16** Za 22:17; Kum 32:35
[h]**38:17** Za 37:24; 38:7; Ay 6:10
[i]**38:18** Law 26:40; Ay 31:33; Za 32:5; Mit 28:13; 2Kor 7:9
[j]**38:19** Za 18:17; 25:19; 35:19
[k]**38:20** Mwa 44:4; Yn 3:12; 1Pet 3:13; Za 54:5; 59:10; 119:23; 1Yn 3:12
[l]**38:21** Za 22:1, 11; 27:9; 71:18; 119:8; 10:1; 35:22; 71:12
[m]**38:22** Za 22:19; 40:13; 1Nya 16:35; Kut 15:2; Isa 12:2
[n]**39:1** 1Fal 2:4; Kol 4:5; Ebr 2:1; Ay 1:22; 6:24; Yak 1:26; 3:2; Za 34:13; 119:9, 59; Mit 4:26, 27; 20:11
[o]**39:2** Za 6:3; 25:17; 39:9; 77:4; 31:10; Ay 31:34
[p]**39:3** Yer 20:9; Lk 24:32; Za 1:2; 119:15; Yer 5:14; 20:9; 23:29
[q]**39:4** Ay 14:5; 14:2; 7:7; Mwa 47:9

nijalie kujua jinsi maisha yangu
yanavyopita upesi.
5 [a]Umefanya maisha yangu mafupi
kama pumzi;
muda wangu wa kuishi ni kama
hauna thamani kwako.
Maisha ya kila mwanadamu
ni kama pumzi.
6 [b]Hakika kila binadamu ni kama njozi
aendapo huku na huko:
hujishughulisha na mengi lakini ni
ubatili;
anakusanya mali nyingi,
wala hajui ni nani atakayeifaidi.

7 [c]"Lakini sasa Bwana, nitafute nini?
Tumaini langu ni kwako.
8 [d]Niokoe kutoka kwenye makosa
yangu yote,
usinifanye kuwa dhihaka ya
wapumbavu.
9 [e]Nilinyamaza kimya,
sikufumbua kinywa changu,
kwa sababu wewe ndiwe
uliyetenda hili.
10 [f]Niondolee mjeledi wako,
nimeshindwa kwa mapigo ya
mkono wako.
11 [g]Unakemea na kuadhibu wanadamu
kwa ajili ya dhambi zao;
unaharibu utajiri wao kama nondo
aharibuvyo:
kila mwanadamu ni kama pumzi
tu.

12 [h]"Ee BWANA, usikie maombi yangu,
usikie kilio changu unisaidie,
usiwe kiziwi kwa kulia kwangu.
Kwani mimi ninaishi na wewe kama
mgeni,
kama walivyokuwa baba zangu
wote,
13 [i]Tazama mbali nami, ili niweze
kufurahi tena
kabla sijaondoka na nisiwepo
tena."

## Zaburi 40

*Wimbo Wa Sifa*

*Kwa mwimbishaji. Zaburi ya Daudi.*

1 [j]Nilimngoja BWANA kwa saburi,
naye akaniinamia, akasikia kilio
changu.
2 [k]Akanipandisha kutoka shimo la
uharibifu,
kutoka matope na utelezi;
akaiweka miguu yangu juu ya
mwamba
na kunipa mahali imara pa
kusimama.
3 [l]Akaweka wimbo mpya kinywani
mwangu,
wimbo wa sifa kwa Mungu wetu.
Wengi wataona na kuogopa
na kuweka tumaini lao kwa
BWANA.

4 [m]Heri mtu yule amfanyaye BWANA
kuwa tumaini lake,
asiyewategemea wenye kiburi,
wale wenye kugeukia miungu ya
uongo.
5 [n]Ee BWANA Mungu wangu,
umefanya mambo mengi ya ajabu.
Mambo uliyopanga kwa ajili yetu
hakuna awezaye kukuhesabia;
kama ningesema na kuyaelezea,
yangekuwa mengi mno
kuyaelezea.

---

[a]**39:5** Ay 10:20; 7:7; Za 62:9; 90:4; 89:45; 102:23
[b]**39:6** Ay 8:9; 27:17; Mhu 6:12; Lk 12:20; Yak 4:14; 1:11; Za 102:11; 127:2
[c]**39:7** Za 9:18
[d]**39:8** Isa 53:5, 8, 10; 43:28; Kum 28:37; Za 69:7; 51:1, 14; 32:1; 6:4; 79:4; Dan 9:16
[e]**39:9** Za 38:13; Isa 38:15
[f]**39:10** 2Nya 21:14; Eze 7:9; 24:16; Kut 9:3
[g]**39:11** Kum 28:20; Isa 26:16; 51:8; 66:15; Eze 5:15; 2Pet 2:16; Za 94:10; 90:7; Ay 7:7; 13:28; Lk 12:33; Yak 5:2
[h]**39:12** Za 17:1; 1Nya 29:15; Ebr 11:13; Law 25:23; Kum 1:45; 2Fal 20:5; Mwa 23:4; 47:9
[i]**39:13** Ay 10:20, 21
[j]**40:1** Za 37:7; 116:1; 6:9; 31:22; 34:15; 7:15; 145:19
[k]**40:2** Ay 9:31; 30:19; Za 7:15; 69:14; 31:8; 27:5
[l]**40:3** Za 28:7; 52:6; 64:9; Ufu 5:9; Kut 14:31
[m]**40:4** Za 2:12; 34:8; 84:12; 101:5; 4:2; 138:6; Kum 31:20; Mit 3:34; 16:5; Isa 65:5; 1Pet 5:5
[n]**40:5** Kum 4:34; Isa 55:8; Za 75:1; 105:5; 136:4; 139:18; 71:15; 139:15

6 [a]Dhabihu na sadaka hukuvitaka,
lakini umefungua masikio yangu;[b]
sadaka za kuteketezwa na sadaka za dhambi
hukuzihitaji.
7 [c]Ndipo niliposema, "Mimi hapa, nimekuja:
imeandikwa kunihusu katika kitabu.
8 [d]Ee Mungu wangu,
natamani kuyafanya mapenzi yako;
sheria yako iko ndani ya moyo wangu."

9 [e]Nimehubiri haki katika kusanyiko kubwa,
sikufunga mdomo wangu,
Ee BWANA, kama ujuavyo.
10 [f]Sikuficha haki yako moyoni mwangu;
ninasema juu ya uaminifu wako na wokovu wako.
Sikuficha upendo wako na kweli yako
mbele ya kusanyiko kubwa.

11 [g]Ee BWANA, usizuilie huruma zako,
upendo wako na kweli yako daima vinilinde.
12 [h]Kwa maana taabu zisizo na hesabu zimenizunguka,
dhambi zangu zimenikamata, hata nisiweze kuona.
Zimekuwa nyingi kuliko nywele za kichwa changu,
nao moyo unazimia ndani yangu.

13 [i]Ee BWANA, uwe radhi kuniokoa;
Ee BWANA, njoo hima unisaidie.
14 [j]Wote wanaotafuta kuuondoa uhai wangu,
waaibishwe na kufadhaishwa;
wote wanaotamani kuangamizwa kwangu,
warudishwe nyuma kwa aibu.
15 [k]Wale waniambiao, "Aha! Aha!"
wafadhaishwe na iwe aibu yao.
16 [l]Lakini wote wakutafutao
washangilie na kukufurahia,
wale wapendao wokovu wako siku zote waseme,
"BWANA atukuzwe!"

17 [m]Lakini bado mimi ni maskini na mhitaji;
Bwana na anifikirie.
Wewe ndiwe msaada wangu na Mwokozi wangu;
Ee Mungu wangu, usikawie.

## Zaburi 41

*Maombi Ya Mtu Mgonjwa*

*Kwa mwimbishaji. Zaburi ya Daudi.*

1 [n]Heri mtu yule anayemjali mnyonge,
BWANA atamwokoa wakati wa shida.
2 [o]BWANA atamlinda na kuyahifadhi maisha yake,
atambariki katika nchi
na hatamwacha katika tamaa ya adui zake.
3 [p]BWANA atamtegemeza awapo mgonjwa kitandani,
atamwinua kutoka kitandani mwake.

[a]**40:6** 1Sam 15:22; Isa 1:11; Hos 6:6; Yer 6:20; Mt 9:13; Amo 5:22; Kut 21:6; Za 50:8; 51:16
[b]6 Au: bali mwili uliniandalia.
[c]**40:7** Ay 19:23; Yn 5:39; Yer 36:2; 45:1; Eze 2:9; Lk 24:44; Mdo 10:43; Ebr 10:7
[d]**40:8** Mt 26:39; Yn 4:34; Ebr 10:5-7; Kum 6:6; Yer 15:16; Rum 7:22; Ay 22:22; 23:12
[e]**40:9** Za 22:25, 31; 139:2; Yos 22:22
[f]**40:10** Za 89:1; 22:22; Mdo 20:20; Flp 3:9; Rum 1:16, 17
[g]**40:11** Zek 1:12; Za 26:3; 61:7; 43:3; Mit 20:28
[h]**40:12** Za 25:17; 38:4; 65:3; 69:4; 73:26
[i]**40:13** Za 22:19; 38:22
[j]**40:14** 1Sam 20:1; Es 9:2; Za 35:26; 35:4
[k]**40:15** Za 35:21
[l]**40:16** Kum 4:29; 1Nya 28:9; Za 9:10; 119:2; 9:2; 35:27
[m]**40:17** Neh 5:19; Mk 10:21; Za 86:1; 109:22; 144:3; 20:2; 18:2; 119:60
[n]**41:1** Kum 14:29; Ay 24:4; Za 25:17; Mit 14:21; Mk 10:21
[o]**41:2** Za 12:5; 32:7; 71:20; 119:88, 159; 138:7; 143:1; 37:22; Ezr 9:9; Kum 6:24
[p]**41:3** Za 6:6; 2Fal 1:4; 2Sam 13:5

4 [a]Nilisema, "Ee BWANA nihurumie,
niponye, maana nimekutenda
dhambi wewe."
5 [b]Adui zangu wanasema kwa hila,
"Lini atakufa, na jina lake
litokomee kabisa."
6 [c]Kila anapokuja mtu kunitazama,
huzungumza uongo,
huku moyo wake hukusanya
masingizio;
kisha huondoka na kuyasambaza
huku na huko.

7 [d]Adui zangu wote hunong'onezana
dhidi yangu,
hao huniwazia mabaya sana,
wakisema,
8 [e]"Ugonjwa mbaya sana umempata,
kamwe hatainuka tena kitandani
mwake."
9 [f]Hata rafiki yangu wa karibu
niliyemwamini,
yule aliyekula chakula changu
ameniinulia kisigino chake.

10 [g]Lakini wewe, Ee BWANA,
nihurumie,
ukaniinue tena, ili niweze
kuwalipiza kisasi.
11 [h]Najua kwamba wapendezwa nami,
kwa kuwa adui yangu hanishindi.
12 [i]Katika uadilifu wangu
unanitegemeza
na kuniweka kwenye uwepo wako
milele.

13 [j]Msifuni BWANA, Mungu wa Israeli,
tangu milele na hata milele.
Amen na Amen.

## KITABU CHA PILI

*(Zaburi 42–72)*

### Zaburi 42

*Maombi Ya Mtu Aliye Uhamishoni*

*Kwa mwimbishaji. Utenzi wa wana wa Kora.*

1 [k]Kama vile ayala aoneavyo shauku
vijito vya maji,
ndivyo nafsi yangu ikuoneavyo
shauku, Ee Mungu.
2 [l]Nafsi yangu inamwonea Mungu kiu,
Mungu aliye hai.
Ni lini nitaweza kwenda kukutana
na Mungu?
3 [m]Machozi yangu yamekuwa chakula
changu
usiku na mchana,
huku watu wakiniambia mchana
kutwa,
"Yuko wapi Mungu wako?"
4 [n]Mambo haya nayakumbuka
ninapoimimina nafsi yangu:
Jinsi nilivyokuwa nikienda na umati
wa watu,
nikiongoza maandamano kuelekea
kwenye nyumba ya Mungu,
kwa kelele za shangwe na za
shukrani
katikati ya umati uliosherehekea.

---

[a]**41:4** Za 6:2; 9:13; Kum 32:39; Za 51:4
[b]**41:5** Za 38:12
[c]**41:6** Za 12:2; 101:7; Mt 5:11; Mit 26:24; Law 19:16
[d]**41:7** Za 71:10
[e]**41:8** 2Fal 1:4
[f]**41:9** Oba 1:7; Yn 13:18; 2Sam 15:12; Ay 19:14, 19; Hes 30:2; Lk 22:21; Za 55:20; 89:34; Mt 26:23
[g]**41:10** Za 3:3; 9:13; 2Sam 3:39
[h]**41:11** Hes 14:8; Za 25:2
[i]**41:12** Za 21:6; 61:7; 34:15; 25:21; 18:35; 37:17; 63:8; Ay 4:7; Mdo 2:38

[j]**41:13** Mwa 24:27; Za 72:18, 19; 89:52; 106:48
[k]**42:1** Ay 19:27; Yoe 1:20; Za 18:33; 119:131; Kum 10:7
[l]**42:2** Za 43:4; 143:6; 84:7; 63:1; Yos 3:10; 1The 1:9; Yn 7:37; Rum 9:26; 1Sam 14:19; Mt 16:16; 9:26
[m]**42:3** Ay 3:24; Mik 7:10; Za 79:10; 115:2; Yoe 2:17
[n]**42:4** 1Sam 1:15; Isa 2:2; 30:29; Yon 2:9; Ezr 3:13; Yos 6:5; Za 35:18; 109:30; 55:14; 122:1; 95:2; 100:4; 147:7

[5] [a]Ee nafsi yangu, kwa nini
unasononeka?
Kwa nini unafadhaika hivyo ndani
yangu?
Weka tumaini lako kwa Mungu,
kwa sababu bado nitamsifu,
Mwokozi wangu na [6] [b]Mungu
wangu.

Nafsi yangu inasononeka ndani
yangu;
kwa hiyo nitakukumbuka
kutoka nchi ya Yordani,
katika vilele vya Hermoni,
kutoka Mlima Mizari.
[7] [c]Kilindi huita kilindi,
katika ngurumo za maporomoko
ya maji yako;
mawimbi yako yote pamoja na
viwimbi
vimepita juu yangu.

[8] [d]Mchana BWANA huelekeza upendo
wake,
usiku wimbo wake uko nami:
maombi kwa Mungu wa uzima
wangu.

[9] [e]Ninamwambia Mungu Mwamba
wangu,
"Kwa nini umenisahau?
Kwa nini niendelee kuomboleza,
nikiwa nimeonewa na adui?"
[10] [f]Mifupa yangu inateseka kwa
maumivu makali
adui zangu wanaponidhihaki,
wakiniambia mchana kutwa,
"Yuko wapi Mungu wako?"

[11] [g]Ee nafsi yangu, kwa nini
unasononeka?
Kwa nini unafadhaika hivyo ndani
yangu?
Weka tumaini lako kwa Mungu,
kwa sababu bado nitamsifu,
Mwokozi wangu na Mungu
wangu.

## Zaburi 43

*Maombi Ya Mtu Aliyeko Uhamishoni Yanaendelea*

[1] [h]Ee Mungu unihukumu,
nitetee dhidi ya taifa lisilomcha
Mungu,
niokoe na watu wadanganyifu na
waovu.
[2] [i]Wewe ni Mungu ngome yangu.
Kwa nini umenikataa?
Kwa nini niendelee kuomboleza,
nikiwa nimeonewa na adui?
[3] [j]Tuma hima nuru yako na kweli
yako
na viniongoze;
vinilete mpaka mlima wako
mtakatifu,
mpaka mahali unapoishi.
[4] [k]Ndipo nitakwenda madhabahuni pa
Mungu,
kwa Mungu, furaha yangu na
shangwe yangu.
Nitakusifu kwa kinubi,
Ee Mungu, Mungu wangu.

[5] [l]Ee nafsi yangu, kwa nini
unasononeka?
Kwa nini unafadhaika hivyo ndani
yangu?
Weka tumaini lako kwa Mungu,
kwa sababu bado nitamsifu
Mwokozi wangu na Mungu
wangu.

---

[a]**42:5** Mao 3:20; Mt 26:38; Za 9:1; 38:6; 77:3; 25:5; 71:14; 56:3, 11; 18:46; Ay 20:2; Isa 50:10
[b]**42:6** Za 43:5; 63:6; 7:11; Mwa 13:10; Hes 13:29; Kum 3:8; 4:48
[c]**42:7** Eze 7:26; Mwa 1:2; 7:11; Za 69:2; Yon 2:3
[d]**42:8** Za 57:3; 16:7; 133:3; Mhu 5:18; 8:15; Kum 28:8
[e]**42:9** Za 18:31; 10:11; 35:14; 106:42; 9:13; 43:2; Ay 20:19
[f]**42:10** Za 89:51; 119:42; 44:16; 6:2; 102:8; Kum 32:27
[g]**42:11** Za 43:5
[h]**43:1** Amu 6:31; Za 25:20; 36:3; 109:2; 7:8
[i]**43:2** Za 44:9; 74:1; 88:14; 89:38; 35:14; 42:9; 28:7; Isa 26:4
[j]**43:3** Za 2:6; 3:4; 27:1; 26:3; 25:5; 2Sam 15:25
[k]**43:4** Za 42:2; 26:6; 84:3; 21:6; 16:3; Mwa 4:21
[l]**43:5** Za 42:5, 6, 11

## Zaburi 44

*Kuomba Ulinzi Wa Mungu*

*Kwa mwimbishaji. Utenzi wa wana wa Kora.*

1 [a]Ee Mungu, tumesikia kwa masikio yetu,
baba zetu wametueleza
yale uliyotenda katika siku zao,
siku za kale.
2 [b]Kwa mkono wako uliwafukuza mataifa
na ukawapanda baba zetu,
uliangamiza mataifa
na kuwastawisha baba zetu.
3 [c]Sio kwa upanga wao waliipata nchi,
wala si mkono wao uliwapatia ushindi;
ilikuwa ni kitanga cha mkono wako wa kuume,
na nuru ya uso wako,
kwa kuwa uliwapenda.

4 [d]Wewe ni mfalme wangu na Mungu wangu,
unayeamuru ushindi kwa Yakobo.
5 [e]Kwa uwezo wako tunawasukuma nyuma watesi wetu;
kwa jina lako tunawakanyaga adui zetu.
6 [f]Siutumaini upinde wangu,
upanga wangu hauniletei ushindi;
7 [g]bali wewe unatupa ushindi juu ya adui zetu,
unawaaibisha watesi wetu.
8 [h]Katika Mungu wetu tunajivuna mchana kutwa,
nasi tutalisifu jina lako milele.

[a]**44:1** 2Sam 7:22; 1Nya 17:20; Yer 26:11; Amu 6:13; Kum 32:7; Ay 37:23
[b]**44:2** Kut 15:17; Kum 7:1; Yos 10:42; 3:10; Mdo 7:45; Isa 60:21; Amu 4:23; 2Nya 14:13; Za 80:9; Yer 32:23
[c]**44:3** Yos 24:12; Kut 15:16; Za 78:54; 77:15; 79:11; 89:10, 15; Isa 40:10; 52:10; 63:5; Kum 4:37
[d]**44:4** Za 24:7; 5:2; 21:5; 74:12
[e]**44:5** Yos 23:5; Za 60:12; 108:13; Dan 8:10
[f]**44:6** Za 33:16; Hos 1:7; Mwa 48:22
[g]**44:7** Kum 20:4; Ay 8:2
[h]**44:8** 1Kor 1:3; Rum 2:17; Za 34:2; 52:1; 30:12; 2Kor 10:17

9 [i]Lakini sasa umetukataa na kutudhili,
wala huendi tena na jeshi letu.
10 [j]Umetufanya turudi nyuma mbele ya adui,
nao watesi wetu wametuteka nyara.
11 [k]Umetuacha tutafunwe kama kondoo
na umetutawanya katika mataifa.
12 [l]Umewauza watu wako kwa fedha kidogo,
wala hukupata faida yoyote kwa mauzo yao.

13 [m]Umetufanya lawama kwa jirani zetu,
dharau na dhihaka kwa wale wanaotuzunguka.
14 [n]Umetufanya kuwa mithali miongoni mwa mataifa,
mataifa hutikisa vichwa vyao.
15 [o]Fedheha yangu iko mbele yangu mchana kutwa,
na uso wangu umejaa aibu tele,
16 [p]kwa ajili ya dhihaka ya wale wanaonilaumu na kunitukana,
kwa sababu ya adui, ambaye anatamani kulipiza kisasi.

17 [q]Hayo yote yametutokea,
ingawa tulikuwa hatujakusahau
wala hatujaenda kinyume na agano lako.

[i]**44:9** Kum 8:3; 31:17; Za 43:2; 107:39; 108:11; Isa 5:15; Yos 7:12
[j]**44:10** Law 26:17; Amu 2:14; Kum 28:25
[k]**44:11** Yer 12:3; 32:37; Law 26:33; Zek 2:6; Kum 4:27; Eze 6:8; Lk 21:24; Za 9:11; 60:1; 2Fal 17:6
[l]**44:12** Kum 32:30; Isa 50:1; 52:3; Yer 15:13
[m]**44:13** 2Nya 29:8; Isa 30:3; Yer 25:9; 42:18; 44:8; Kum 28:37; Mik 2:6; Za 79:4; 80:6; 89:41; Eze 23:32
[n]**44:14** 1Fal 9:7; 2Fal 19:21
[o]**44:15** Mwa 30:23; 2Nya 32:21; Za 35:26; 34:5
[p]**44:16** Za 42:10; 10:13; 55:3; 74:10; 1Sam 18:25; Yer 11:19; Rum 12:19
[q]**44:17** Kum 6:12; 32:18; Mit 3:1; Dan 9:13; Za 119:16, 61, 153, 176

18 [a]Mioyo yetu ilikuwa haijarudi
nyuma;
nyayo zetu zilikuwa hazijaiacha
njia yako.
19 [b]Lakini ulituponda na kutufanya
makao ya mbweha,
na ukatufunika kwa giza nene.

20 [c]Kama tungalikuwa tumelisahau jina
la Mungu wetu
au kunyooshea mikono yetu kwa
mungu mgeni,
21 [d]je, Mungu hangaligundua hili,
kwa kuwa anazijua siri za moyo?
22 [e]Hata hivyo kwa ajili yako tunauawa
mchana kutwa;
tumehesabiwa kama kondoo wa
kuchinjwa.

23 [f]Amka, Ee BWANA! Kwa nini
unalala?
Zinduka! Usitukatae milele.
24 [g]Kwa nini unauficha uso wako
na kusahau taabu na mateso yetu?

25 [h]Tumeshushwa hadi mavumbini,
miili yetu imegandamana na
ardhi.
26 [i]Inuka na utusaidie,
utukomboe kwa sababu ya upendo
wako usio na mwisho.

[a]**44:18** Za 119:51, 157
[b]**44:19** 2Nya 14:13; Za 51:8; Isa 43:12; Ay 30:29; 3:5
[c]**44:20** Kum 32:18; Amu 4:7; Isa 43:12; Kut 20:3; Yer 5:12
[d]**44:21** 1Sam 16:7; 1Fal 8:39; Yn 2:25; Mit 15:11; Yer 12:3; 17:10; Ay 31:14; Za 139:1; Mhu 12:14; Mdo 1:24; Ufu 2:23; Rum 2:16; Ebr 4:12
[e]**44:22** Yer 11:19; 12:3; Isa 53:7; Rum 8:36
[f]**44:23** Za 7:6; 78:65; 59:5; 74:1; 77:7
[g]**44:24** Mao 5:20
[h]**44:25** Za 119:25
[i]**44:26** Za 102:13; 26:11; 12:5; 6:4; Hes 10:25

## Zaburi 45

*Wimbo Wa Arusi Ya Kifalme*

*Kwa mwimbishaji. Mtindo wa utenzi wa "Yungiyungi." Utenzi wa wana wa Kora. Wimbo wa arusi.*

1 Moyo wangu umesisimuliwa na
jambo jema
ninapomsimulia mfalme mabeti
yangu;
ulimi wangu ni kalamu ya
mwandishi stadi.

2 [j]Wewe ni bora kuliko watu wengine
wote
na midomo yako imepakwa
neema,
kwa kuwa Mungu amekubariki
milele.
3 [k]Jifunge upanga wako pajani mwako,
ee mwenye nguvu,
jivike fahari na utukufu.
4 [l]Katika fahari yako, songa mbele
kwa ushindi,
kwa ajili ya kweli, unyenyekevu
na haki,
mkono wako wa kuume na
uonyeshe matendo ya kutisha.
5 [m]Mishale yako mikali na ichome
mioyo ya adui za mfalme,
mataifa na yaanguke chini ya
nyayo zako.
6 [n]Ee Mungu, kiti chako cha enzi
kitadumu milele na milele,
fimbo ya utawala wa haki
itakuwa fimbo ya utawala wa
ufalme wako.
7 [o]Unaipenda haki na kuchukia uovu;
kwa hiyo Mungu, Mungu wako,

[j]**45:2** Lk 4:22; Za 21:6
[k]**45:3** Kum 32:41; Ufu 1:16; Za 21:5; 149:6; 2Sam 1:19; Ay 40:10
[l]**45:4** Ufu 6:2; Sef 2:3; Za 21:8; 65:5; 66:3; Kum 4:34
[m]**45:5** Kum 32:23; Hes 24:8; Isa 50:10; Za 56:3, 11; 9:13; 92:9; Mao 3:24
[n]**45:6** Mwa 21:33; Mao 5:13; Za 93:2; Isa 9:6, 7; Ebr 1:8
[o]**45:7** Za 33:5; 11:5; 2:2; 23:5; Ebr 1:9; Eze 7:26; Isa 45:1; 61:1; Yn 20:17; Mt 3:15; Zek 4:14

amekuweka juu ya wenzako,
kwa kukupaka mafuta ya furaha.
8 [a]Mavazi yako yote yana harufu nzuri
ya manemane, udi na mdalasini;
kutoka kwenye majumba ya kifalme
yaliyopambwa kwa pembe za
ndovu,
sauti za vinanda vya nyuzi
zinakufanya ufurahi.
9 [b]Binti za wafalme ni miongoni
mwa wanawake wako
waheshimiwa;
kuume kwako yupo bibi arusi
malkia aliyevaa dhahabu ya
Ofiri.

10 [c]Sikiliza, ewe binti, fikiri na utege
sikio:
Sahau watu wako na nyumba ya
baba yako.
11 [d]Mfalme ameshangazwa na uzuri
wako;
mheshimu, kwa kuwa yeye ni
bwana wako.
12 [e]Binti wa Tiro atakuletea zawadi,
watu wenye utajiri watatafuta
upendeleo wako.

13 [f]Utukufu wote una binti mfalme
katika chumba chake;
vazi lake limefumwa kwa nyuzi za
dhahabu.
14 [g]Anaongozwa kwa mfalme,
akiwa amevalia mavazi
yaliyotariziwa,
mabikira wenzake wanamfuata
na wanaletwa kwako.
15 [h]Wanaingizwa ndani kwa shangwe
na furaha,
na kuingia katika jumba la
mfalme.

16 [i]Wana wenu watachukua nafasi za
baba zenu,
mtawafanya wakuu katika nchi
yote.
17 [j]Nitadumisha kumbukumbu lako
katika vizazi vyote,
kwa hiyo mataifa watakusifu
milele na milele.

## Zaburi 46

*Mungu Yuko Pamoja Nasi*

*Kwa mwimbishaji. Zaburi ya wana wa Kora. Mtindo wa alamothi.*

1 [k]Mungu kwetu sisi ni kimbilio na
nguvu,
msaada utakaoonekana tele wakati
wa mateso.
2 [l]Kwa hiyo hatutaogopa, hata kama
dunia ikiondolewa
nayo milima ikiangukia moyoni
mwa bahari.
3 [m]Hata kama maji yake yatanguruma
na kuumuka,
milima nayo ikitetemeka kwa
mawimbi yake.

---

[a] **45:8** Kum 28:8; Wim 1:3; 4:10; Mwa 37:25; Hes 24:6; Yn 19:39; Kut 30:24; 1Fal 22:39; Za 144:9; 150:4; Isa 38:20; Mt 27:9
[b] **45:9** Wim 6:8; Isa 62:5; Mwa 10:29; 1Fal 2:19
[c] **45:10** Yer 5:1; Rut 1:11; 1:16; Kum 21:13
[d] **45:11** Mao 2:15; Efe 5:33; Isa 54:5; Za 95:6; Es 1:11
[e] **45:12** Yos 19:29; 1Fal 9:16; 2Nya 9:24
[f] **45:13** Isa 61:10; Kut 39:3; Ufu 19:7, 8
[g] **45:14** Amu 5:30; Es 2:15; Wim 1:3
[h] **45:15** Es 8:17
[i] **45:16** 1Sam 2:8; Za 68:27; 113:8; 1Pet 2:9; Ufu 1:6
[j] **45:17** Isa 11:10; Mal 1:11; Kut 3:15; Ufu 22:5; Za 33:11; 138:4; 119:90; 135:13
[k] **46:1** Za 9:9; 18:1, 6; 25:17; 34:18; 61:3; 37:39; 73:26; 91:2, 9; 142:5; Isa 33:16; Lk 1:54; Yer 16:19; 17:17; Yoe 3:16; Nah 1:7; Mao 3:57; Kum 4:30
[l] **46:2** Mwa 4:7; Za 3:6; 18:7; 97:5; 82:5; Dan 11:19; Hab 3:6; Yer 4:23; Amo 9:5; 8:14; Isa 24:1, 19, 20; 13:13; 54:10; Ufu 6:14; Kut 15:8; Mik 1:4; Nah 1:5
[m] **46:3** Za 93:3; Ufu 19:6; Isa 17:13; Amu 5:5; Yer 5:22; Eze 1:24; Ay 9:26

4 [a]Kuna mto ambao vijito vyake
vinaufurahisha mji wa
Mungu,
mahali patakatifu ambako Aliye
Juu Sana anaishi.
5 [b]Mungu yuko katikati yake,
hautaanguka,
Mungu atausaidia asubuhi na
mapema.
6 [c]Mataifa yanafanya ghasia, falme
zinaanguka,
Yeye huinua sauti yake, dunia
ikayeyuka.

7 [d]BWANA Mwenye Nguvu Zote yu
pamoja nasi,
Mungu wa Yakobo ni ngome yetu.

8 [e]Njooni mkaone kazi za BWANA
jinsi alivyofanya ukiwa katika
nchi.
9 [f]Anakomesha vita hata miisho ya
dunia,
anakata upinde na kuvunjavunja
mkuki,
anateketeza ngao kwa moto.
10 [g]"Tulieni, mjue ya kwamba mimi
ndimi Mungu;
nitatukuzwa katikati ya mataifa,
nitatukuzwa katika dunia."

11 BWANA Mwenye Nguvu Zote yu
pamoja nasi;
Mungu wa Yakobo ni ngome yetu.

## Zaburi 47

*Mtawala Mwenye Enzi Yote*

*Kwa mwimbishaji. Zaburi ya wana wa Kora.*

1 [h]Pigeni makofi, enyi mataifa yote,
mpigieni Mungu kelele za
shangwe!
2 [i]Jinsi gani alivyo wa kutisha,
BWANA Aliye Juu Sana,
Mfalme mkuu juu ya dunia yote!
3 [j]Ametiisha mataifa chini yetu
watu wengi chini ya miguu yetu.
4 [k]Alituchagulia urithi wetu,
fahari ya Yakobo, aliyempenda.

5 [l]Mungu amepaa kwa kelele za
shangwe,
BWANA kwa sauti za tarumbeta.
6 [m]Mwimbieni Mungu sifa, imbeni sifa,
mwimbieni sifa Mfalme wetu,
imbeni sifa.

7 [n]Kwa kuwa Mungu ni mfalme wa
dunia yote,
mwimbieni zaburi za sifa.
8 [o]Mungu anatawala juu ya mataifa,
Mungu ameketi juu ya kiti chake
cha enzi kitakatifu.
9 [p]Wakuu wa mataifa wanakusanyika
kama watu wa Mungu wa
Abrahamu,
kwa kuwa wafalme wa dunia ni mali
ya Mungu;
yeye ametukuka sana.

---

[a]**46:4** Ufu 22:1; Isa 60:14; 8:7; 2Sam 15:25; Ebr 12:22; Za 48:1; 2Nya 6:6; Mwa 14:18
[b]**46:5** Kum 23:14, 15; Isa 12:6; Eze 43:7; Zek 2:5; Za 26:8; 125:1; 1Nya 5:20
[c]**46:6** Ay 12:23; Mt 4:8; Za 68:32; 74:23; 102:22; 29:3; Isa 17:12; 23:11; 13:4, 13; 5:30; 33:3; Eze 26:18
[d]**46:7** 1Sam 1:11; Mwa 21:22; Za 20:1; 18:2
[e]**46:8** Za 66:5; Isa 17:9; 64:10; Dan 9:26; Lk 21:20
[f]**46:9** Isa 2:4; Za 37:15; Isa 22:6; 9:5; Eze 39:9; Hos 2:18
[g]**46:10** Kum 4:35; Isa 2:11; 37:16, 20; 43:11; 45:21; Eze 36:23; 1Fal 18:36, 39; Za 18:46; 100:3

---

[h]**47:1** 2Fal 11:12; Za 33:3
[i]**47:2** Kum 7:21; Mal 1:14; Mwa 14:18; Neh 1:5; Za 2; 6; 48:2; 95:3; Mt 5:35
[j]**47:3** Za 18:39, 47; Isa 14:6
[k]**47:4** Za 2:8; 16:6; 78:55; 1Pet 1:4; Amo 6:8; 8:7
[l]**47:5** Za 68:18; Efe 4:8
[m]**47:6** 2Sam 22:50
[n]**47:7** Zek 14:9, 19; 1Nya 16:7; Kol 3:16; 1Kor 14:15
[o]**47:8** 1Nya 16:31; 1Fal 22:19; Za 9:4; Ufu 4:9
[p]**47:9** Ay 25:2; Za 46:10; 97:9

### Zaburi 48

*Sayuni, Mji Wa Mungu*

*Wimbo. Zaburi ya wana wa Kora.*

1 [a]BWANA ni mkuu, anayestahili
kusifiwa sana,
katika mji wa Mungu wetu,
mlima wake mtakatifu.
2 [b]Ni mzuri katika kuinuka kwake juu
sana,
furaha ya dunia yote.
Kama vilele vya juu sana vya Safoni[c]
ni Mlima Sayuni,
mji wa Mfalme Mkuu.
3 [d]Mungu yuko katika ngome zake;
amejionyesha mwenyewe kuwa
ngome yake.

4 [e]Wakati wafalme walipounganisha
nguvu,
waliposonga mbele pamoja,
5 [f]walimwona nao wakashangaa,
wakakimbia kwa hofu.
6 [g]Kutetemeka kuliwashika huko,
maumivu kama ya mwanamke
mwenye utungu wa kuzaa.
7 [h]Uliwaangamiza kama meli za
Tarshishi
zilizovunjwa na upepo wa
mashariki.

8 [i]Kama tulivyokuwa tumesikia,
ndivyo tulivyoona
katika mji wa BWANA Mwenye
Nguvu Zote,
katika mji wa Mungu wetu:
Mungu ataufanya uwe salama
milele.

9 [j]Ee Mungu, hekaluni mwako
tunatafakari upendo wako
usiokoma.
10 [k]Ee Mungu, kama jina lako lilivyo,
sifa zako zinafika hadi miisho ya
dunia,
mkono wako wa kuume umejazwa
na haki.
11 [l]Mlima Sayuni unashangilia,
vijiji vya Yuda vinafurahi
kwa sababu ya hukumu zako.

12 [m]Tembeeni katika Sayuni,
uzungukeni mji,
hesabuni minara yake;
13 [n]yatafakarini vyema maboma yake,
angalieni ngome zake,
ili mpate kusimulia habari zake
kwa kizazi kijacho.
14 [o]Kwa kuwa huyu Mungu ni Mungu
wetu milele na milele;
atakuwa kiongozi wetu hata
mwisho.

### Zaburi 49

*Upumbavu Wa Kutegemea Mali*

*Kwa mwimbishaji. Zaburi ya wana wa Kora.*

1 [p]Sikieni haya, enyi mataifa yote,
sikilizeni, ninyi wote mkaao dunia
hii.
2 [q]Wakubwa kwa wadogo,
matajiri na maskini pamoja:

---

[a]**48:1** 2Sam 22:4; Mik 4:1; Yer 10:6; 31:23; Za 86:10; 96:4; 99:2; 135:5; 147:5; 46:4; 87:1; 18:3; 2:6; 1Nya 16:25; Kum 33:19; Isa 2:2; 11:9; 32:16; Zek 8:3; Oba 1:17; Dan 9:16
[b]**48:2** Isa 14:13; Za 2:6; 50:2; Mao 2:15; Eze 16:14; 20:6; Yos 13:17; Mt 5:35; Yer 3:19
[c]2 Safoni inaweza ikawa na maana ya mlima mtakatifu au upande wa kaskazini.
[d]**48:3** Za 122:7; 18:2
[e]**48:4** 2Sam 10:1-19
[f]**48:5** Kut 15:16
[g]**48:6** Ay 4:14; Mwa 3:16
[h]**48:7** Mwa 10:4; 41:6; 1Fal 10:22; 22:48; Eze 27:26
[i]**48:8** Yer 23:6; Mik 4:1; Zek 8:13; 14:11; Isa 2:2
[j]**48:9** Za 39:3; 6:4
[k]**48:10** Kut 6:3; Isa 11:12; 24:16; 42:10; 49:6; Yos 7:9; 1Sam 2:10; Za 22:27; 100:1; 65:5; 98:3; Mal 1:1
[l]**48:11** Za 97:8
[m]**48:12** Neh 3:1
[n]**48:13** 2Sam 20:15; Isa 26:1; Mao 2:8; Hab 2:1; Za 78:6; 71:18; 109:13
[o]**48:14** Za 25:5; 73:24; Mit 6:22; Isa 25:9; 49:10; 57:18; 58:11
[p]**49:1** Isa 1:2; Za 33:8; 78:1
[q]**49:2** Za 62:9

3 [a]Kinywa changu kitasema maneno ya hekima,
usemi wa moyo wangu utatoa ufahamu.
4 [b]Nitatega sikio langu nisikilize mithali,
nitafafanua kitendawili kwa zeze:

5 [c]Kwa nini niogope siku mbaya zinapokuja,
wakati wadanganyifu waovu wanaponizunguka,
6 [d]wale wanaotegemea mali zao
na kujivunia utajiri wao mwingi?
7 [e]Hakuna mwanadamu awaye yote
awezaye kuukomboa uhai wa mwingine,
au kumpa Mungu fidia kwa ajili yake.
8 [f]Fidia ya uhai ni gharama kubwa,
hakuna malipo yoyote yanayotosha,
9 [g]ili kwamba aishi milele
na asione uharibifu.

10 [h]Wote wanaona kwamba watu wenye hekima hufa;
wajinga na wapumbavu vivyo hivyo huangamia
na kuwaachia wengine mali zao.
11 [i]Makaburi yao yatabaki kuwa nyumba zao za milele,
makao yao vizazi vyote;
ingawa walikuwa na mashamba
na kuyaita kwa majina yao.

12 [j]Lakini mwanadamu, licha ya utajiri wake, hadumu;
anafanana na mnyama aangamiaye.

13 [k]Hii ndiyo hatima ya wale wanaojitumainia wenyewe,
pia ya wafuasi wao,
waliothibitisha misemo yao.
14 [l]Kama kondoo, wamewekewa kwenda kaburini,[m]
nacho kifo kitawala.
Wanyofu watawatawala asubuhi,
maumbile yao yataozea kaburini,
mbali na majumba yao makubwa ya fahari.
15 [n]Lakini Mungu atakomboa uhai[o] wangu na kaburi,
hakika atanichukua kwake.

16 Usitishwe mtu anapotajirika,
fahari ya nyumba yake inapoongezeka,
17 [p]kwa maana hatachukua chochote atakapokufa,
fahari yake haitashuka pamoja naye.
18 [q]Ingawa alipokuwa akiishi alijihesabu kuwa heri,
na wanadamu wanakusifu unapofanikiwa,
19 [r]atajiunga na kizazi cha baba zake,
ambao hawataona kamwe nuru ya uzima.

20 [s]Mwanadamu mwenye utajiri bila ufahamu
ni kama wanyama waangamiao.

---

[a] **49:3** Za 37:30; 119:130
[b] **49:4** Za 33:2; 78:2; 1Sam 16:16; Mit 1:6; Eze 12:22; 16:44; 18:2, 3; Hes 12:8; Lk 4:23
[c] **49:5** Za 23:4; 27:1
[d] **49:6** Yer 48:7; Za 10:3; 73:12; Ay 22:25; 36:19
[e] **49:7** Mt 16:26
[f] **49:8** Hes 35:31; Mt 16:26; Ay 36:18
[g] **49:9** Za 22:29; 89:48; 16:10; Ebr 9:27
[h] **49:10** Mhu 2:16, 18, 21; Za 92:6; 94:8; Ay 27:17; Lk 12:20
[i] **49:11** Mk 5:3; Lk 8:27; Za 106:31; Kum 3:14
[j] **49:12** Ay 14:2
[k] **49:13** Lk 12:20
[l] **49:14** Yer 43:11; Isa 14:2; Hes 16:30; Eze 31:14; Mal 4:3; Ay 21:13; Ufu 2:26; 1Kor 6:2; Za 9:17; 55:15; Dan 7:18, 22; Lk 22:30; 2Tim 2:12
[m] 14 Kaburini hapa ina maana ya Sheol kwa Kiebrania, yaani Kuzimu.
[n] **49:15** Za 56:13; Hos 13:14; Mwa 5:24
[o] 15 Au: nafsi.
[p] **49:17** 1Tim 6:7; Za 17:14
[q] **49:18** Za 10:6; Lk 12:19
[r] **49:19** Mwa 15:15; Ay 33:30
[s] **49:20** Mit 16:16; Mhu 3:19-21

## Zaburi 50

*Ibada Ya Kweli*

*Zaburi ya Asafu.*

1 [a]Mwenye Nguvu, Mungu, BWANA,
asema na kuiita dunia,
tangu mawio ya jua
hadi mahali pake liendapo kutua.
2 [b]Kutoka Sayuni, penye uzuri
mkamilifu,
Mungu anaangaza.
3 [c]Mungu wetu anakuja na hatakaa
kimya,
moto uteketezao unamtangulia,
akiwa amezungukwa na tufani
kali.
4 [d]Anaziita mbingu zilizo juu,
na nchi, ili aweze kuwahukumu
watu wake:
5 [e]"Nikusanyieni watu wangu
waliowekwa wakfu,
waliofanya agano nami kwa
dhabihu."
6 [f]Nazo mbingu zinatangaza haki
yake,
kwa maana Mungu mwenyewe ni
hakimu.

7 [g]"Sikieni, enyi watu wangu, nami
nitasema,
ee Israeli, nami nitashuhudia dhidi
yenu:
Mimi ndimi Mungu, Mungu wenu.
8 [h]Sikukemei kwa sababu ya dhabihu
zako,
au sadaka zako za kuteketezwa,
ambazo daima ziko mbele zangu.
9 [i]Sina haja ya fahali wa banda lako,
au mbuzi wa zizi lako.
10 [j]Kwa maana kila mnyama wa
msituni ni wangu,
na pia makundi ya mifugo juu ya
vilima elfu.
11 [k]Ninamjua kila ndege mlimani,
nao viumbe wa kondeni ni wangu.
12 [l]Kama ningekuwa na njaa,
nisingewaambia ninyi,
kwa maana ulimwengu ni wangu,
pamoja na vyote vilivyomo ndani
yake.
13 Je, mimi hula nyama ya mafahali
au kunywa damu ya mbuzi?
14 [m]Toa sadaka za shukrani kwa Mungu,
timiza nadhiri zako kwake Yeye
Aliye Juu Sana,
15 [n]na uniite siku ya taabu;
nami nitakuokoa, nawe
utanitukuza."

16 [o]Lakini kwake mtu mwovu, Mungu
asema:

"Una haki gani kunena sheria zangu
au kuchukua agano langu
midomoni mwako?
17 [p]Unachukia mafundisho yangu
na kuyatupa maneno yangu
nyuma yako.
18 [q]Unapomwona mwizi, unaungana
naye,
unapiga kura yako pamoja na
wazinzi.

---

[a]**50:1** Yos 22:22; Za 113:3
[b]**50:2** Za 2:6; 48:2; Mao 2:15; Kum 33:2
[c]**50:3** Isa 30:28; 42:14; 64:12; 29:6; 65:6; Za 18:8; 107:25; 96:13; 83:15; 147:18; Ay 37:9; Yn 1:4; Nah 1:3
[d]**50:4** Kum 4:26; 31:26; Isa 1:2; Ebr 10:30; Mik 6:1, 2
[e]**50:5** Kum 7:6; Za 18:25; Kut 24:7; 1Kor 6:2; 2Nya 6:11; Isa 13:3; 1The 3:13; Ebr 8:6; Yud 14; Mwa 24:7; Isa 59:20, 21
[f]**50:6** Za 19:1; Ay 9:15; Mwa 16:5
[g]**50:7** Ebr 2:4; Kut 20:2; Za 48:14
[h]**50:8** 2Sam 22:16; Za 40:6
[i]**50:9** Hes 32:16; Law 1:5; 16:5; Mdo 17:25; Mik 6:6; Isa 43:23
[j]**50:10** Za 104:20, 24; Isa 56:9; Mik 5:8
[k]**50:11** Mt 6:26; Za 8:7; 80:13
[l]**50:12** Kut 19:5; Kum 10:14; Ay 3:11; Za 24:1; 1Kor 10:26
[m]**50:14** Ezr 1:4; Za 27:6; 66:13; 76:11; 7:8; Hes 30:2
[n]**50:15** Zek 13:9; Isa 55:6; 58:9; Za 4:1; 3:7; 81:7; 69:17; 142:2; 86:7; 22:23; 107:6; Yak 5:13; Yn 15:8
[o]**50:16** Za 25:10; Isa 29:13
[p]**50:17** 1Fal 14:9; Mit 1:22; 5:12, 13; Rum 2:21; 2The 2:10-12
[q]**50:18** Rum 1:32; 1Tim 5:22; Ay 22:15

19 [a]Unakitumia kinywa chako kwa mabaya
na kuuongoza ulimi wako kwa hila.
20 [b]Wanena daima dhidi ya ndugu yako
na kumsingizia mwana wa mama yako.
21 [c]Mambo haya unayafanya, nami nimekaa kimya,
ukafikiri Mimi nami ni kama wewe.
Lakini nitakukemea
na kuweka mashtaka mbele yako.

22 [d]"Yatafakarini haya, ninyi mnaomsahau Mungu,
ama sivyo nitawararua vipande vipande,
wala hapatakuwepo na yeyote wa kuwaokoa:
23 [e]Atoaye dhabihu za shukrani ananiheshimu mimi,
naye aiandaa njia yake
ili nimwonyeshe wokovu wa Mungu."

## Zaburi 51

*Kuomba Msamaha*

*Kwa mwimbishaji. Zaburi ya Daudi. Baada ya kukemewa na nabii Nathani kwa kuzini na Bathsheba.*

1 [f]Ee Mungu, unihurumie,
kwa kadiri ya upendo wako usiokoma,
kwa kadiri ya huruma yako kuu,
uyafute makosa yangu.
2 [g]Unioshe na uovu wangu wote
na unitakase dhambi yangu.

3 [h]Kwa maana ninajua makosa yangu,
na dhambi yangu iko mbele yangu daima.
4 [i]Dhidi yako, wewe peke yako, nimetenda dhambi
na kufanya yaliyo mabaya machoni pako,
ili uthibitike kuwa wa kweli unenapo,
na kuwa na haki utoapo hukumu.
5 [j]Hakika mimi nilizaliwa mwenye dhambi,
mwenye dhambi tangu nilipotungwa mimba kwa mama yangu.
6 [k]Hakika wewe wapendezwa na kweli itokayo moyoni,
ndani sana ya moyo wangu wanifundisha hekima.

7 [l]Nioshe kwa hisopo, nami nitakuwa safi,
unisafishe, nami nitakuwa mweupe kuliko theluji.
8 [m]Unipe kusikia furaha na shangwe,
mifupa uliyoiponda na ifurahi.
9 [n]Ufiche uso wako usizitazame dhambi zangu,
na uufute uovu wangu wote.

10 [o]Ee Mungu, uniumbie moyo safi,
uifanye upya roho ya uthabiti ndani yangu.

---

[a]**50:19** Za 10:7; 36:3; 52:2; 101:7
[b]**50:20** Mt 10:21
[c]**50:21** Isa 57:11, 16; 62:1; 42:14; 64:12; 50:2; Mhu 8:11; Za 6:1; 18:15; 85:5; 76:6; 104:7; Rum 2:4
[d]**50:22** Ay 8:13; Mik 5:8; Isa 17:10; Kum 32:39
[e]**50:23** Za 85:13; 98:3; 9:14; 91:16; Isa 52:10
[f]**51:1** 2Sam 24:14; 12:13; Za 39:8; 86:15; 25:7; 119:88; 9:13; Neh 4:5; 9:27; Isa 63:7; Kol 2:14; 2Nya 6:23; Mdo 3:19
[g]**51:2** Rum 3:3; Yer 2:22; 13:27; Mdo 22:16; Mit 20:30; Isa 4:4; Ebr 9:14; Zek 13:1; Ufu 1:5; 1Kor 6:11; Eze 13:1; 36:25; Mt 23:25, 26; 1Yn 1:7, 9
[h]**51:3** Isa 59:12; Za 32:5
[i]**51:4** 1Sam 15:24; Mwa 20:6; Lk 15:21; Rum 3:4
[j]**51:5** Law 5:2; Ay 5:7; 14:4; Rum 5:12; Yn 3:6
[k]**51:6** Ay 9:4; 34:32; Za 119:66; 143:10
[l]**51:7** Eze 36:25; Hes 19:6; Zek 13:1; Kut 12:22; Ebr 9:19; Isa 4:4; 1:19; 43:25; 44:22
[m]**51:8** Isa 35:10; Kut 12:46; Yer 33:11; Yoe 1:16
[n]**51:9** Yer 16:17; Zek 4:10; 2Sam 12:13
[o]**51:10** Za 24:4; 78:37; Mt 5:8; Mdo 15:9; Eze 11:19; 18:31; 36:26; Mit 20:9; Yer 13:27; Efe 2:10

[11] [a]Usinitupe kutoka mbele zako
wala kuniondolea Roho wako
Mtakatifu.
[12] [b]Unirudishie tena furaha ya wokovu
wako,
unipe roho ya utii, ili initegemeze.

[13] [c]Ndipo nitakapowafundisha wakosaji
njia zako,
na wenye dhambi watakugeukia
wewe.
[14] [d]Ee Mungu, Mungu uniokoaye,
niokoe na hatia ya kumwaga
damu,
nao ulimi wangu utaimba juu ya
haki yako.
[15] [e]Ee BWANA, fungua midomo yangu,
na kinywa changu kitatangaza sifa
zako.
[16] [f]Wewe hupendezwi na dhabihu, au
ningaliiileta,
hufurahii sadaka za kuteketezwa.
[17] [g]Bali dhabihu za Mungu ni roho
iliyovunjika,
moyo uliovunjika wenye toba,
Ee Mungu, hutaudharau.

[18] [h]Kwa wema wa radhi yako uifanye
Sayuni istawi,
ukazijenge upya kuta za
Yerusalemu.
[19] Hapo ndipo kutakapokuwa na
dhabihu za haki,
sadaka nzima za kuteketezwa za
kukupendeza sana,
pia mafahali watatolewa
madhabahuni mwako.

## Zaburi 52

*Hukumu Ya Mungu*

*Kwa mwimbishaji. Utenzi wa Daudi. Baada ya Doegi, Mwedomu kumwendea Sauli na kumjulisha kuwa: "Daudi amekwenda nyumbani kwa Ahimeleki."*

[1] [i]Ewe jitu, mbona unajivunia ubaya?
Kwa nini unajivuna mchana
kutwa,
wewe ambaye ni fedheha mbele za
Mungu?
[2] [j]Ulimi wako hupanga mashauri
mabaya ya maangamizi.
Ni kama wembe mkali, ninyi
mfanyao hila.
[3] [k]Unapenda mabaya kuliko mema,
uongo kuliko kusema kweli.
[4] [l]Unapenda kila neno lenye kudhuru,
ewe ulimi wenye hila!

[5] [m]Hakika Mungu atakushusha chini
kwa maangamizi ya milele:
atakunyakua na kukuondoa kwa
nguvu
kutoka hema yako,
atakung'oa kutoka nchi ya walio
hai.
[6] [n]Wenye haki wataona na kuogopa,
watamcheka, wakisema,
[7] [o]"Huyu ni yule mtu ambaye
hakumfanya Mungu kuwa ngome
yake,
bali alitumainia wingi wa utajiri
wake,
na akawa hodari kwa
kuwaangamiza wengine!"

---

[a]**51:11** Za 27:9; 138:8; 71:9; 106:3; Kut 33:15; Mwa 4:14; Isa 63:10; Eze 36:27; Efe 4:30; Rum 8:9
[b]**51:12** Ay 33:26; Za 110:3; 18:35; Rum 8:15; 2Kor 3:17
[c]**51:13** Kut 33:13; Za 1:1; Mdo 9:21-22; Ay 33:27
[d]**51:14** 2Sam 12:9; Za 5:8; 22:5; 39:8; 68:20; 88:1; 35:28; 71:15
[e]**51:15** Kut 4:15
[f]**51:16** 1Sam 15:22
[g]**51:17** Mit 15:8; Hag 2:14; Mt 11:29
[h]**51:18** Za 69:35; 147:2; 102:16; Zek 1:16-17; Isa 14:32; 44:26; 51:3; 51:19; Kum 33:19; Mal 3:3

[i]**52:1** Za 10:3; 44:8; 94:4; 1Sam 21:7
[j]**52:2** Za 5:9; 59:7; Hes 6:5; Mit 12:18
[k]**52:3** Kut 10:10; Za 58:3; 1Sam 12:25; Amo 5:14, 15; Yn 3:20; Ufu 21:8; Yer 9:4, 5
[l]**52:4** Za 5:9; 10:7; 109:2; 120:2, 3; Mit 10:31; 12:19
[m]**52:5** Kum 28:63; 29:28; Ay 28:13; 40:12; Isa 22:19; Mit 2:22; Eze 17:24
[n]**52:6** Ay 22:19; Za 58:10
[o]**52:7** 2Sam 22:3; Za 49:6; Mk 10:23; Mit 11:28; Ay 31:24, 25

*Neema Ya Mungu*

8 [a]Lakini mimi ni kama mti wa
mzeituni
unaostawi katika nyumba ya
Mungu,
nautegemea upendo wa Mungu
usiokoma
milele na milele.
9 [b]Nitakusifu milele kwa yale
uliyoyatenda,
nitatumaini jina lako, kwa kuwa
jina lako ni jema.
Nitakusifu mbele ya watakatifu
wako.

## Zaburi 53

*Uovu Wa Wanadamu*

**(Zaburi 14)**

*Kwa mwimbishaji. Mtindo wa mahalathi. Utenzi wa Daudi.*

1 [c]Mpumbavu anasema moyoni
mwake,
"Hakuna Mungu."
Wameharibika, na njia zao ni za
uovu kabisa,
hakuna hata mmoja atendaye
mema.

2 [d]Mungu anawachungulia wanadamu
chini
kutoka mbinguni
aone kama wako wenye akili,
wowote wanaomtafuta Mungu.
3 [e]Kila mmoja amegeukia mbali,
wameharibika wote pamoja,
hakuna atendaye mema.
Naam, hakuna hata mmoja!

4 [f]Je, watendao mabaya kamwe
hawatajifunza:
wale ambao huwala watu wangu
kama watu walavyo mkate,
hao ambao hawamwiti Mungu?
5 [g]Hapo waliingiwa na hofu kuu,
ambapo hapakuwa cha
kutetemesha.
Mungu alitawanya mifupa ya wale
waliokushambulia;
uliwaaibisha, kwa sababu Mungu
aliwadharau.

6 Laiti wokovu wa Israeli ungalikuja
kutoka Sayuni!
Wakati Mungu arejeshapo
wafungwa wa watu wake,
Yakobo na ashangilie, Israeli na
afurahi!

## Zaburi 54

*Kuomba Ulinzi Wa Mungu Kutokana Na Adui*

*Kwa mwimbishaji. Na ala za nyuzi za uimbaji. Utenzi wa Daudi. Wakati Wazifu walimwendea Sauli na kumjulisha, "Je, Daudi hajifichi miongoni mwetu?"*

1 [h]Ee Mungu uniokoe kwa jina lako,
unifanyie hukumu kwa uwezo
wako.
2 [i]Ee Mungu, sikia maombi yangu,
usikilize maneno ya kinywa
changu.

3 [j]Wageni wananishambulia,
watu wakatili wanayatafuta
maisha yangu,
watu wasiomjali Mungu.

4 [k]Hakika Mungu ni msaada wangu,
Bwana ndiye anayenitegemeza.

5 [l]Mabaya na yawarudie wale
wanaonisingizia,
kwa uaminifu wako uwaangamize.

---

[a]**52:8** Ufu 11:4; Za 1:3; 6:4; 13:5; 54:6
[b]**52:9** Ay 7:6; Za 16:3; 30:12; 25:3; 54:6; Kum 7:6
[c]**53:1** Za 107:17; 74:22; 10:4; Mit 10:23; Rum 3:10
[d]**53:2** Za 33:13; 82:5; Yer 4:22; 8:8; 2Nya 15:2
[e]**53:3** Rum 3:10-12; Mhu 7:29
[f]**53:4** Yer 4:22
[g]**53:5** Law 26:17; Eze 6:5; 2Fal 17:20; 23:14; Za 141:7; Mao 5:22; Yer 6:30; 14:19; 8:1; Ay 8:22
[h]**54:1** 1Sam 24:15; 20:1; 2Nya 20:6
[i]**54:2** Za 4:1; 5:1; 55:1
[j]**54:3** Za 36:1; 86:14; 18:48; 140:1, 4, 11; 1Sam 20:1
[k]**54:4** 1Nya 5:20; Za 20:2; 18:35; Isa 41:10; Ebr 13:6; Rum 8:31, 32
[l]**54:5** Kum 32:35; Isa 42:3; Mit 24:12; Za 89:49; 94:23

6 [a]Nitakutolea dhabihu za hiari;
Ee BWANA, nitalisifu jina lako
kwa kuwa ni vyema.
7 Kwa maana ameniokoa katika shida
zangu zote,
na macho yangu yamewatazama
adui zangu kwa ushindi.

## Zaburi 55

*Maombi Ya Mtu Aliyesalitiwa Na Rafiki*

*Kwa mwimbishaji. Na ala za uimbaji. Utenzi wa Daudi.*

1 [b]Ee Mungu, sikiliza maombi yangu,
wala usidharau hoja yangu.
2 [c]Nisikie na unijibu.
Mawazo yangu yananisumbua na
nimehangaishwa
3 [d]kwa sauti ya adui,
kwa kukaziwa macho na waovu,
kwa sababu wananiletea mateso juu
yangu
na kunitukana kwa hasira zao.

4 [e]Moyo wangu umejaa uchungu,
hofu ya kifo imenishambulia.
5 [f]Woga na kutetemeka
vimenizunguka,
hofu kuu imenigharikisha.
6 Nilisema, "Laiti ningekuwa na
mbawa za njiwa!
Ningeruka niende mbali
kupumzika.
7 [g]Ningalitorokea mbali sana
na kukaa jangwani,
8 [h]ningaliharakisha kwenda mahali pa
salama,
mbali na tufani kali na dhoruba."

9 [i]Ee BWANA, uwatahayarishe waovu
na uwachanganyishie semi zao,
maana nimeona jeuri na ugomvi
mjini.
10 [j]Usiku na mchana wanazunguka juu
ya kuta zake,
uovu na dhuluma vimo ndani
yake.
11 [k]Nguvu za uharibifu zinatenda kazi
mjini,
vitisho na uongo haviondoki
mitaani mwake.

12 Kama aliyenitukana ni adui yangu,
ningevumilia,
kama mtu mwovu angejiinua dhidi
yangu,
ningejificha asinione.
13 [l]Kumbe ni wewe, mwenzangu,
mshiriki na rafiki yangu wa
karibu,
14 [m]ambaye awali tulifurahia ushirika
mzuri,
tulipokuwa tukienda na umati
hekaluni mwa Mungu.

15 [n]Kifo na kiwajie adui zangu ghafula,
na washuke kuzimu wangali hai,
kwa maana uovu upo ndani yao.

16 Lakini ninamwita Mungu,
naye BWANA huniokoa.
17 [o]Jioni, asubuhi na adhuhuri
ninalia kwa huzuni,
naye husikia sauti yangu.
18 [p]Huniokoa nikawa salama katika vita
vilivyopangwa dhidi yangu,
ingawa watu wengi hunipinga.

---

[a] **54:6** Law 7:12, 16; Ezr 1:4; Za 27:6; 44:8; 52:9; 138:2; 142:7; 145:1; 69:30
[b] **55:1** Za 27:9; Mao 3:56
[c] **55:2** 1Sam 1:15-16; Za 4:1; 77:3; 86:6-7; 142:2
[d] **55:3** 2Sam 16:6-8; 17:9; Za 143:3; 44:16; 71:11
[e] **55:4** Ay 18:11; Za 6:3; 102:3-5; Yn 12:27; Mt 26:37, 38; 2Kor 1:8-10
[f] **55:5** Ay 4:14; Eze 7:18; 2Kor 7:15; Isa 21:4; Kum 28:67; Yer 46:5; 49:5
[g] **55:7** 1Sam 23:14
[h] **55:8** Za 31:20; 77:18; Isa 4:6; 25:4; 28:2; 29:6; 32:2
[i] **55:9** Mwa 4:17; 11:9; Mdo 2:4; Za 11:5; Isa 59:6; Yer 6:7; Eze 7:11; Hab 1:3
[j] **55:10** 1Pet 5:8
[k] **55:11** Za 5:9; 10:7
[l] **55:13** 2Sam 15:12
[m] **55:14** Mdo 1:16-17; Za 42:4
[n] **55:15** Za 64:7; 49:14; Mit 6:5; Isa 29:5; 47:9, 11; 1The 5:3; Hes 16:30
[o] **55:17** Za 141:2; 88:13; 92:2; 5:3; Mdo 3:1; 10:9; 10:3, 30; Lk 18:1; Dan 6:10
[p] **55:18** 2Nya 32:7

19 [a]Mungu anayemiliki milele,
atawasikia na kuwaadhibu,
watu ambao hawabadilishi njia zao,
wala hawana hofu ya Mungu.

20 [b]Mwenzangu hushambulia rafiki zake,
naye huvunja agano lake.
21 [c]Mazungumzo yake ni laini kama siagi,
hata hivyo vita vimo moyoni mwake.
Maneno yake ni mororo kuliko mafuta,
hata hivyo ni upanga mkali uliofutwa.

22 [d]Mtwike BWANA fadhaa zako,
naye atakutegemeza,
hatamwacha kamwe mwenye haki wake aanguke.
23 [e]Lakini wewe, Ee Mungu,
utawashusha waovu katika shimo la uharibifu.
Wenye kiu ya kumwaga damu na wenye hila,
hawataishi nusu ya siku zao.

Lakini mimi ninakutumaini wewe.

## Zaburi 56

*Kumtumaini Mungu*

*Kwa mwimbishaji. Mtindo wa "Njiwa mkimya wa mbali." Utenzi wa Daudi. Baada ya kukamatwa na Wafilisti huko Gathi.*

1 [f]Ee Mungu unihurumie, maana watu wananifuatia vikali;
mchana kutwa wanazidisha mashambulizi yao.
2 [g]Wasingiziaji wangu wananifuatia mchana kutwa,
wengi wananishambulia kwa kiburi chao.

3 [h]Wakati ninapoogopa,
nitakutumaini wewe.
4 [i]Katika Mungu, ambaye neno lake ninalisifu,
katika Mungu ninatumaini; sitaogopa.
Mwanadamu apatikanaye na kufa,
atanitenda nini?

5 [j]Mchana kutwa wanayageuza maneno yangu,
siku zote wanapanga shauri la kunidhuru.
6 [k]Wananifanyia hila, wanajificha,
wanatazama hatua zangu,
wakiwa na shauku ya kuutoa uhai wangu.

7 [l]Wasiepuke kwa vyovyote,
Ee Mungu, katika hasira yako yaangushe mataifa.
8 [m]Andika maombolezo yangu,
orodhesha machozi yangu katika gombo lako:
je, haya hayapo katika kumbukumbu zako?

9 [n]Ndipo adui zangu watarudi nyuma
ninapoita msaada.
Kwa hili nitajua kwamba Mungu
yuko upande wangu.
10 Katika Mungu, ambaye neno lake ninalisifu,
katika BWANA, ambaye neno lake ninalisifu,

---

[a] **55:19** Kum 33:27; Za 29:10; 78:59; 36:1; 64:4; Kut 15:18
[b] **55:20** Za 7:4; 41:9
[c] **55:21** Za 59:7; 57:4; 12:2; 64:3; Ufu 1:16; Mit 5:3; 6:24; 12:18
[d] **55:22** 1Pet 5:7; Za 15:5; 18:35; 112:6; 21:7; 37:24; Mt 6:25-34
[e] **55:23** Za 5:6; 11:1; 9:15; 73:18; 94:13; 25:2; 30:3; 56:3; Isa 14:15; Eze 28:8; Lk 8:31; Ay 15:32
[f] **56:1** Za 6:2; 57:1-3; 17:9; 31:9
[g] **56:2** Za 57:3; 35:1, 25; 124:3
[h] **56:3** 1Sam 30:6; 2Nya 20:3; Za 55:4-5, 23
[i] **56:4** Ebr 13:5, 6; 13:6; Za 27:1; 118:6; Mt 10:28
[j] **56:5** Za 41:7; 2Pet 3:16
[k] **56:6** Mk 3:6; Za 59:3; 94:21; 71:16; 17:11; Mdo 4:27, 28
[l] **56:7** Mt 19:5; Eze 17:15; Rum 2:3; Ebr 12:25; Za 36:12; 55:23
[m] **56:8** 2Fal 20:5; Isa 4:3; Dan 7:10; 12:1; Mal 3:16
[n] **56:9** Rum 8:31; Za 9:3; 102:2; Hes 14:8; Kum 31:6

11 katika Mungu ninatumaini,
sitaogopa.
Mwanadamu anaweza kunitenda
nini?

12 [a]Ee Mungu, nina nadhiri kwako,
nitakutolea wewe sadaka zangu za
shukrani.
13 [b]Kwa kuwa umeniokoa toka kwenye
mauti
na miguu yangu kwenye kujikwaa,
ili niweze kuenenda mbele za Mungu
katika nuru ya uzima.

## Zaburi 57

*Kuomba Msaada*

*Kwa mwimbishaji. Mtindo wa "Usiharibu!" Utenzi wa Daudi. Baada ya kumponyoka Sauli pangoni.*

1 [c]Unihurumie, Ee Mungu,
unihurumie,
kwa maana nafsi yangu
inakukimbilia.
Chini ya uvuli wa mbawa zako
nitakimbilia
mpaka maafa yapite.

2 [d]Namlilia Mungu Aliye Juu Sana,
Mungu atimizaye makusudi yake
kwangu.
3 [e]Hutumana kutoka mbinguni na
kuniokoa,
akiwakemea wale wanaonifuatilia
vikali;
Mungu huutuma upendo wake na
uaminifu wake.

4 [f]Niko katikati ya simba,
nimelala katikati ya wanyama
wenye njaa kuu:
watu ambao meno yao ni mikuki
na mishale,
ambao ndimi zao ni panga kali.

5 [g]Ee Mungu, utukuzwe juu ya
mbingu,
utukufu wako na uenee duniani
kote.

6 [h]Waliitegea miguu yangu nyavu,
nikainamishwa chini na dhiki.
Wamechimba shimo katika njia
yangu,
lakini wametumbukia humo wao
wenyewe.

7 [i]Ee Mungu, moyo wangu ni thabiti;
nitaimba na kusifu kwa moyo
wangu wote.
8 [j]Amka, nafsi yangu!
Amka, kinubi na zeze!
Nitayaamsha mapambazuko.

9 Nitakusifu wewe, Ee BWANA,
katikati ya mataifa;
nitaimba habari zako, katikati ya
jamaa za watu.
10 [k]Kwa maana upendo wako ni mkuu,
waenea hadi mbinguni,
uaminifu wako unazifikia anga.

11 [l]Ee Mungu, utukuzwe juu mbinguni,
utukufu wako na uwe duniani
pote.

## Zaburi 58

*Mungu Kuwaadhibu Waovu*

*Kwa mwimbishaji. Mtindo wa "Usiharibu!" Utenzi wa Daudi.*

1 Enyi watawala, je, kweli mwanena
kwa haki?
Je, mnahukumu kwa unyofu
miongoni mwa watu?
2 [m]La, mioyoni mwenu mnatunga
udhalimu,
na mikono yenu hupima jeuri
duniani.

---

[a]**56:12** Za 50:14; 116:14-16
[b]**56:13** Za 30:3; 33:19; 49:15; 86:13; 107:20; 116:8; Ay 33:30
[c]**57:1** Isa 26:20
[d]**57:2** Za 138:8
[e]**57:3** Za 18:9, 16; 69:14; 142:5, 7; 56:1; 25:10; 40:11; 115:1
[f]**57:4** Za 35:17; 55:21; 64:3; Mit 30:14
[g]**57:5** Za 108:5
[h]**57:6** Es 6:13; Za 31:4; 9:15; 140:5; 7:15; 38:6; 10:9; 145:14; Mit 28:10; Mhu 10:8
[i]**57:7** Za 112:7; 108:1
[j]**57:8** Za 33:2; 149:3; 150:3; Amu 5:12
[k]**57:10** Za 36:5; 108:4
[l]**57:11** Za 8:1; 149:3; 150:3; Amu 5:12
[m]**58:2** Za 74:20; Isa 10:1; Mt 15:19; Lk 6:38

3 [a]Waovu ni wapotovu tangu kuzaliwa
kwao,
toka tumboni mwa mama zao
ni wakaidi na husema uongo.
4 [b]Sumu yao ni kama sumu ya nyoka,
kama ile ya fira ambaye ameziba
masikio yake,
5 [c]ambaye hatasikia sauti ya
kutumbuiza ya mwaguzi,
hata kama mganga angecheza kwa
ustadi kiasi gani.

6 [d]Ee Mungu, yavunje meno katika
vinywa vyao;
Ee BWANA, vunja meno makali ya
hao simba!
7 [e]Na watoweke kama maji yapitayo
kwa kasi,
wavutapo pinde zao, mishale yao
na iwe butu.
8 [f]Kama konokono ayeyukavyo
akitembea,
kama mtoto aliyezaliwa akiwa
mfu,
wasilione jua.
9 [g]Kabla vyungu vyenu havijapata
moto wa kuni za miiba,
zikiwa mbichi au kavu,
waovu watakuwa
wamefagiliwa mbali.
10 [h]Wenye haki watafurahi waonapo
wakilipizwa kisasi,
watakapochovya nyayo zao katika
damu ya waovu.
11 [i]Ndipo wanadamu watasema,
"Hakika utulivu wa wenye haki
bado una thawabu,
hakika kuna Mungu ahukumuye
dunia."

## Zaburi 59

*Kuomba Ulinzi Wa Mungu*

*Kwa mwimbishaji. Mtindo wa "Usiharibu!" Utenzi wa Daudi. Wakati Sauli alipotuma wapelelezi nyumbani mwa Daudi ili wamuue.*

1 [jk]Ee Mungu, uniokoe na adui zangu,
unilinde kutokana na hao
wanaoinuka dhidi yangu.
2 [l]Uniponye na watu watendao
mabaya,
uniokoe kutokana na wamwagao
damu.

3 [m]Tazama wanavyonivizia!
Watu wakali wananifanyia hila,
ingawa Ee BWANA, mimi sijakosea
wala kutenda dhambi.
4 [n]Sijatenda kosa; hata hivyo wako
tayari kunishambulia.
Inuka unisaidie, uone hali yangu
mbaya!
5 [o]Ee BWANA Mwenye Nguvu Zote,
Mungu wa Israeli!
Zinduka uyaadhibu mataifa yote,
usionyeshe huruma kwa wasaliti.

6 [p]Hurudi wakati wa jioni,
wakibweka kama mbwa,
wakiuzurura mji.

---

[a]**58:3** Za 51:5
[b]**58:4** Hes 21:6; Za 140:4
[c]**58:5** Za 81:11; Mhu 10:1; Yer 8:17
[d]**58:6** Ay 4:10; Za 3:7
[e]**58:7** Law 26:36; Ay 11:16; Za 11:2; 57:4; 64:3
[f]**58:8** Isa 13:7; Ay 3:16
[g]**58:9** Za 118:12; Mhu 7:6; Ay 7:10; Mit 10:25
[h]**58:10** Ay 22:19; Kum 32:42; 32:35; Yer 11:20; Mit 10:11; Rum 12:17-21; Za 18:47; 7:9; 91:8; 68:23; Ufu 18:20
[i]**58:11** Mwa 4:12, 13; 15:1; Za 128:2; Lk 6:23; Ufu 2:23; Rum 2:6-11; 14:12; Ay 34:11; Mhu 5:8; Yer 32:19; Eze 7:27
[j]**59:1** Za 82:2
[k]**59:1** Za 143:9; 20:1
[l]**59:2** Za 14:4; 36:12; 53:4; 92:7; 94:16; 26:9; 139:19; Mit 29:10
[m]**59:3** Za 56:6; 1Sam 26:18
[n]**59:4** Za 13:3; 119:3; Mt 5:11
[o]**59:5** Za 69:6; 80:4; 84:8; 44:23; 9:5; Isa 10:3; Yer 18:23; Dan 4:35
[p]**59:6** Za 22:16

7 [a]Tazama yale wanayotema kutoka
vinywa vyao,
hutema upanga kutoka midomo
yao,
nao husema, “Ni nani
atakayetusikia?”
8 [b]Lakini wewe, BWANA, uwacheke;
unayadharau mataifa hayo yote.

9 [c]Ee nguvu yangu, ninakutazama
wewe,
wewe, Ee Mungu, ndiwe ngome
yangu,
10 Mungu wangu unipendaye.

Mungu atanitangulia,
naye atanifanya niwachekelee
wale wanaonisingizia.
11 [d]Lakini usiwaue, Ee BWANA, ngao
yetu,
au sivyo watu wangu watasahau.
Katika uwezo wako wafanye
watangetange
na uwashushe chini.
12 [e]Kwa ajili ya dhambi za vinywa
vyao,
kwa ajili ya maneno ya midomo
yao,
waache wanaswe katika kiburi
chao.
Kwa ajili ya laana na uongo
wanaotamka,
13 [f]wateketeze katika ghadhabu,
wateketeze hadi wasiwepo tena.
Ndipo itakapofahamika katika
miisho ya dunia
kwamba Mungu anatawala juu ya
Yakobo.

14 Hurudi jioni,
wakibweka kama mbwa,
wakiuzurura mji.
15 [g]Wanatangatanga wakitafuta
chakula,
wasipotosheka hubweka kama
mbwa.
16 [h]Lakini mimi nitaziimba nguvu zako,
asubuhi nitaimba juu ya upendo
wako;
kwa maana wewe ndiwe ngome
yangu
na kimbilio langu wakati wa
shida.
17 [i]Ee uliye Nguvu zangu, ninakuimbia
sifa.
Wewe, Ee Mungu, ndiwe ngome
yangu,
Mungu unipendaye.

## Zaburi 60

*Kuomba Kuokolewa*

*Kwa mwimbishaji. Mtindo wa “Shushani Eduthi.” Utenzi wa Daudi wa kufundisha. Wakati alipopigana na Waaramu kutoka Aramu-Naharaimu na Aramu-Soba, naye Yoabu akarudi nyuma na kuwaua Waedomu 12,000 katika Bonde la Chumvi.*

1 [j]Ee Mungu, umetukataa na kutokea
ghafula juu yetu,
umekasirika: sasa turejeshe upya!
2 Umetetemesha nchi na kuipasua;
uiponye mavunjiko yake, kwa
maana inatetemeka.
3 [k]Umewaonyesha watu wako nyakati
za kukata tamaa;
umetunywesha mvinyo
unaotuyumbisha.

4 [l]Kwa wale wanaokucha wewe,
umewainulia bendera,
ili iweze kutwekwa dhidi ya
upinde.

---

[a]**59:7** Za 55:21; 94:4; Mit 10:32; 12:23; 15:2, 28; Ay 22:13
[b]**59:8** Za 2:4; 37:13; Mit 1:26
[c]**59:9** Za 18:1; 9:9; 18:2; 62:2; 71:3
[d]**59:11** Kum 4:9; 6:12; Za 3:3; 84:9; 89:10; 106:27; 144:6; Isa 33:3; Mwa 4:12, 13
[e]**59:12** Za 10:7; 64:8; Mit 10:14; 12:13; Isa 2:12; 5:15; Sef 3:11
[f]**59:13** Za 83:18; 104:35
[g]**59:15** Ay 15:23
[h]**59:16** Za 5:3; 88:13; 101:1; 108:1; 1Sam 2:10; 2Sam 22:3; Kum 4:30
[i]**59:17** Za 59:1
[j]**60:1** 2Sam 5:20; Za 18:7; 44:9; 79:5; 80:3; 60:2; 2Nya 7:14
[k]**60:3** Za 71:20; 75:8; Isa 29:9; 51:17; 63:6; Yer 25:16; Zek 12:2; Ufu 14:10
[l]**60:4** Isa 5:26; 11:10, 12; 18:3

5 [a]Tuokoe na utusaidie kwa mkono
wako wa kuume,
ili wale uwapendao wapate
kuokolewa.
6 [b]Mungu amenena kutoka patakatifu
pake:
“Nitaigawa Shekemu kwa ushindi
na kulipima Bonde la Sukothi.
7 [c]Gileadi ni yangu na Manase ni
yangu;
Efraimu ni kofia yangu ya chuma,
nayo Yuda ni fimbo yangu ya
utawala.
8 [d]Moabu ni sinia langu la kunawia,
juu ya Edomu natupa kiatu
changu;
nashangilia kwa kushindwa kwa
Ufilisti.”

9 Ni nani atakayenipeleka hadi mji
wenye ngome?
Ni nani atakayeniongoza hadi
nifike Edomu?
10 [e]Ee Mungu, si ni wewe uliyetukataa
sisi,
na hutoki tena na majeshi yetu?
11 [f]Tuletee msaada dhidi ya adui,
kwa maana msaada wa
mwanadamu haufai kitu.
12 [g]Kwa msaada wa Mungu tutapata
ushindi,
naye atawaponda adui zetu.

## Zaburi 61

*Kuomba Ulinzi*

*Kwa mwimbishaji. Kwa ala za nyuzi za uimbaji. Zaburi ya Daudi.*

1 [h]Ee Mungu, sikia kilio changu,
usikilize maombi yangu.
2 [i]Kutoka miisho ya dunia ninakuita,
ninaita huku moyo wangu
unadhoofika;
uniongoze kwenye mwamba
ule ulio juu kuliko mimi.
3 [j]Kwa kuwa umekuwa kimbilio langu,
ngome imara dhidi ya adui.

4 [k]Natamani kukaa hemani mwako
milele,
na kukimbilia chini ya uvuli wa
mbawa zako.
5 [l]Ee Mungu, kwa kuwa umesikia
nadhiri zangu,
umenipa urithi wa wale
wanaoliogopa jina lako.

6 [m]Mwongezee mfalme siku za maisha
yake,
miaka yake kwa vizazi vingi.
7 [n]Yeye na atawazwe kwenye kiti cha
enzi mbele za Mungu milele;
amuru upendo wako na uaminifu
wako vimlinde.

8 [o]Ndipo daima nitaliimbia sifa jina
lako
na kuzitimiza nadhiri zangu siku
baada ya siku.

## Zaburi 62

*Mungu Kimbilio La Pekee*

*Kwa mwimbishaji. Mtindo wa Yeduthuni. Zaburi ya Daudi.*

1 [p]Kwa Mungu peke yake nafsi yangu
inapata pumziko;
wokovu wangu watoka kwake.

---

[a]**60:5** Ay 40:14; Kum 33:12; Za 108:6
[b]**60:6** Mwa 12:6; 33:17; Za 89:35; Yos 13:27
[c]**60:7** Yos 13:31; Hes 34:19; Mwa 41:52; 49:10; Kum 33:17
[d]**60:8** 2Sam 8:1
[e]**60:10** Yos 7:12; Za 44:9
[f]**60:11** Za 146:3; Mit 3:5
[g]**60:12** 1Nya 19:13; Ay 40:12; Za 44:5
[h]**61:1** Za 64:1; 4:1; 86:6
[i]**61:2** Za 6:2; 18:2; 31:2; 94:22; 1Tim 2:8
[j]**61:3** Za 9:9; 46:1; 62:7; 59:9; Mit 18:10
[k]**61:4** Kum 32:11; Mt 23:37; Ufu 3:12; Za 15:1; 23:6
[l]**61:5** Hes 30:2; Kut 6:3; Neh 1:11; Mt 6:9; Za 56:12; 102:15; Isa 59:19; 1Kor 3:21-23; Kum 33:9
[m]**61:6** 1Fal 3:14; Za 21:4
[n]**61:7** Za 40:11; 41:12; Lk 22:69; Efe 1:20; Kol 3:1; Lk 1:32
[o]**61:8** Kut 15:1; Hes 30:2; Kum 23:21; Za 7:17; 30:4; 56:12
[p]**62:1** Za 5:3

2 [a]Yeye peke yake ndiye mwamba
wangu na wokovu wangu;
yeye ni ngome yangu, sitatikisika
kamwe.

3 [b]Mtamshambulia mtu hata lini?
Je, ninyi nyote mtamtupa chini,
ukuta huu ulioinama na uzio huu
unaotikisika?
4 [c]Walikusudia kikamilifu
kumwangusha
toka mahali pake pa fahari;
wanafurahia uongo.
Kwa vinywa vyao hubariki,
lakini ndani ya mioyo yao hulaani.

5 [d]Ee nafsi yangu, upumzike, kwa
Mungu peke yake,
tumaini langu latoka kwake.
6 Yeye peke yake ndiye mwamba
wangu na wokovu wangu;
ndiye ngome yangu, sitatikisika.
7 [e]Wokovu wangu na heshima yangu
viko kwa Mungu,
ndiye mwamba wangu wenye
nguvu
na kimbilio langu.
8 [f]Enyi watu, mtumainini yeye wakati
wote,
miminieni mioyo yenu kwake,
kwa kuwa Mungu ni kimbilio letu.

9 [g]Binadamu wa ngazi ya chini ni
pumzi tu,
nao wa ngazi ya juu ni uongo tu;
wakipimwa kwenye mizani, si
chochote;
wote kwa pamoja ni pumzi tu.
10 [h]Usitumainie vya udhalimu
wala usijivune kwa vitu vya wizi;
ingawa utajiri wako utaongezeka,
usiviwekee moyo wako.

11 [i]Jambo moja Mungu amelisema,
mambo mawili nimeyasikia:
kwamba, Ee Mungu,
wewe una nguvu,
12 [j]na kwamba, Ee BWANA,
wewe ni mwenye upendo.
Hakika utampa kila mtu thawabu
kwa kadiri ya alivyotenda.

## Zaburi 63

*Shauku Kwa Ajili Ya Uwepo Wa Mungu*

*Zaburi ya Daudi. Wakati alipokuwa katika Jangwa la Yuda.*

1 [k]Ee Mungu, wewe ni Mungu wangu,
nakutafuta kwa moyo wote;
nafsi yangu inakuonea kiu,
mwili wangu unakuonea wewe
shauku,
katika nchi kame na iliyochoka
mahali ambapo hapana maji.

2 [l]Nimekuona katika mahali patakatifu
na kuuona uwezo wako na
utukufu wako.
3 [m]Kwa sababu upendo wako ni bora
kuliko uhai,
midomo yangu itakuadhimisha.
4 [n]Nitakusifu siku zote za maisha
yangu,
na kwa jina lako nitainua mikono
yangu.
5 [o]Nafsi yangu itatoshelezwa
kama kwa wingi wa vyakula;
kwa midomo iimbayo
kinywa changu kitakusifu wewe.

---

[a]**62:2** Kut 15:2; Za 18:31; 89:26; 59:9; Ay 29:18
[b]**62:3** Isa 30:13
[c]**62:4** Za 28:3; 55:21
[d]**62:5** Mik 7:7, 10; Za 62:1
[e]**62:7** Za 61:3
[f]**62:8** Isa 26:4; 1Sam 1:15; Za 37:5; 42:4; Mt 26:36-46
[g]**62:9** Za 49:2; Ay 7:7; Isa 40:15
[h]**62:10** Za 12:5; Isa 61:8; 26:4; 1Tim 6:17; Eze 22:29; Nah 3:1; Lk 12:15; Ay 31:25; Mt 19:23, 24; 1Tim 6:6-10; Mk 10:23
[i]**62:11** 1Nya 29:11; Ufu 19:1
[j]**62:12** Za 130:7; 103:8; 86:5; 28:4; Ay 21:31; Mt 16:27; Rum 2:6; 1Kor 3:8; Kol 3:25; 1Pet 1:17
[k]**63:1** Za 42:2; 84:2; 143:6
[l]**63:2** Za 15:1; 27:4; 68:24; Kut 16:7; 1Nya 16:11
[m]**63:3** Isa 30:13; Yn 3:16; Za 36:7; 69:16; 106:45; 109:21
[n]**63:4** Za 28:3; 104:33; 146:2; Isa 38:20; 1Tim 2:8
[o]**63:5** Za 17:15; 36:8; Mt 5:6; Isa 25:6

[6] [a]Kitandani mwangu ninakukumbuka wewe,
ninawaza juu yako makesha yote ya usiku.
[7] [b]Kwa sababu wewe ndiwe msaada wangu,
chini ya uvuli wa mbawa zako naimba.
[8] [c]Nafsi yangu inaambatana nawe,
mkono wako wa kuume hunishika.

[9] [d]Wale wanaotafuta uhai wangu wataharibiwa,
watakwenda chini kwenye vilindi vya dunia.
[10] [e]Watatolewa wafe kwa upanga,
nao watakuwa chakula cha mbweha.

[11] [f]Bali mfalme atafurahi katika Mungu,
wale wote waapao kwa jina la Mungu watamsifu,
bali vinywa vya waongo vitanyamazishwa.

## Zaburi 64

*Kuomba Ulinzi Dhidi Ya Maadui*

*Kwa mwimbishaji. Zaburi ya Daudi.*

[1] [g]Ee Mungu, unisikie ninapoeleza lalamiko langu,
uyahifadhi maisha yangu kutokana na vitisho vya adui.
[2] [h]Unifiche kutokana na shauri la siri la waovu,
kutokana na zile kelele za kundi la watenda mabaya.

[3] [i]Wananoa ndimi zao kama panga
na kuelekeza maneno yao kama mishale ya kufisha.
[4] [j]Hurusha mishale kutoka kwenye mavizio kwa mtu asiye na hatia,
humrushia ghafula bila woga.

[5] [k]Kila mmoja humtia moyo mwenzake katika mipango mibaya;
huzungumza juu ya kuficha mitego yao,
nao husema, “Ni nani ataiona?”
[6] Hufanya shauri baya la dhuluma na kusema,
“Tumebuni mpango mkamilifu!”
Hakika nia na moyo wa mwanadamu vina hila.

[7] Bali Mungu atawapiga kwa mishale,
nao ghafula wataangushwa.
[8] [l]Atageuza ndimi zao wenyewe dhidi yao
na kuwaleta kwenye maangamizi;
wote wawaonao watatikisa vichwa vyao
kwa dharau.

[9] [m]Wanadamu wote wataogopa,
watatangaza kazi za Mungu
na kutafakari yale aliyoyatenda.
[10] [n]Wenye haki na wafurahi katika Bwana,
na wakimbilie kwake;
wanyofu wote wa moyo na wamsifu yeye!

---

[a]**63:6** Kum 6:4-9; Za 119:148; 16:7; 140:5; Mt 14:25
[b]**63:7** Za 27:9; 118:7; Rum 2:12; Isa 26:9
[c]**63:8** Hes 32:12; Hos 6:3; Isa 26:9; Za 41:12
[d]**63:9** Za 40:14; 55:15; 71:20; 95:4; 139:15
[e]**63:10** Yer 18:21; Eze 35:5; Amo 1:11; Mao 5:18
[f]**63:11** Sef 1:5; Isa 19:18; 45:23; 65:16; Ay 5:16; Rum 3:19
[g]**64:1** Za 142:2; 140:1
[h]**64:2** Za 56:6; 59:2; 143:9; Kut 1:10
[i]**64:3** Za 7:13; 58:7; 57:4; 55:21; Isa 49:2
[j]**64:4** Za 10:8; 11:2; 55:19; Ay 9:23
[k]**64:5** Za 91:3; 140:5; 119:110; 141:9; Ay 22:13
[l]**64:8** Mit 12:13; 18:7; 2Fal 10:21; Za 109:25; 59:12; Kum 28:37
[m]**64:9** Za 40:3; Yer 51:10
[n]**64:10** Ay 22:19

## Zaburi 65

*Kusifu Na Kushukuru*

*Kwa mwimbishaji. Zaburi ya Daudi. Wimbo.*

1 [a]Ee Mungu, sifa zakungojea katika
Sayuni;
kwako wewe nadhiri zetu
zitatimizwa.
2 [b]Ewe usikiaye maombi,
kwako wewe watu wote watakuja.
3 [c]Tulipokuwa tumefunikwa kabisa na
dhambi,
wewe ulisamehe makosa yetu.
4 [d]Heri wale uliowachagua
na kuwaleta karibu ili waishi
katika nyua zako!
Tunashibishwa kwa mema ya
nyumba yako,
mema ya Hekalu lako takatifu.

5 [e]Unatujibu kwa matendo ya
kushangaza ya haki,
Ee Mungu Mwokozi wetu,
tumaini la miisho yote ya duniani
na la bahari zilizo mbali sana,
6 [f]uliyeumba milima kwa uwezo wako,
ukiwa umejivika nguvu,
7 [g]uliyenyamazisha dhoruba za bahari,
ngurumo za mawimbi yake,
na ghasia za mataifa.
8 [h]Wale wanaoishi mbali sana
wanaogopa maajabu yako,
kule asubuhi ipambazukiapo
na kule jioni inakofifilia
umeziita nyimbo za furaha.

9 [i]Waitunza nchi na kuinyeshea,
waitajirisha kwa wingi.
Vijito vya Mungu vimejaa maji
ili kuwapa watu nafaka,
kwa maana wewe umeviamuru.
10 [j]Umeilowesha mifereji yake
na kusawazisha kingo zake;
umeilainisha kwa manyunyu
na kuibariki mimea yake.
11 [k]Umeuvika mwaka taji ya baraka,
magari yako yanafurika kwa
wingi.
12 [l]Mbuga za majani za jangwani
umezineemesha;
vilima vimevikwa furaha.
13 [m]Penye nyanda za malisho pamejaa
makundi ya wanyama,
na mabonde yamepambwa kwa
mavuno;
vyote vinashangilia kwa furaha na
kuimba.

## Zaburi 66

*Kusifu Mungu Kwa Ajili Ya Wema Wake*

*Kwa mwimbishaji. Wimbo. Zaburi.*

1 [n]Mpigieni Mungu kelele za shangwe,
dunia yote!
2 [o]Imbeni utukufu wa jina lake;
mpeni sifa zake kwa utukufu!
3 [p]Mwambieni Mungu, “Jinsi gani
yalivyo ya kutisha matendo
yako!
Uwezo wako ni mkuu mno kiasi
kwamba
adui wananyenyekea mbele zako.
4 [q]Dunia yote yakusujudia,
wanakuimbia wewe sifa,
wanaliimbia sifa jina lako.”

---

[a]**65:1** Kum 23:21; Za 2:6; 116:18
[b]**65:2** Za 86:9; Isa 66:23; Lk 11:9, 10
[c]**65:3** Za 40:12; 79:9; Rum 3:25; Ebr 9:14
[d]**65:4** Hes 16:5; Za 33:12; 36:8
[e]**65:5** Kum 4:34; Isa 64:3; Za 107:23; 18:46; 68:19; 85:4; 45:4; 48:10; 106:22
[f]**65:6** Amo 4:13; Isa 51:9; Za 18:1; 93:1
[g]**65:7** Za 139:20; 89:9; 74:23; 2:1; 93:3, 4; 107:29; Mt 8:26; Kum 32:41; Isa 17:12-13
[h]**65:8** Ay 37:5; Za 100:2; 107:22; 126:2; Isa 24:16; 52:9
[i]**65:9** Za 104:14, 24; 68:9, 10; Law 26:4; Mwa 27:28; Kum 32:14
[j]**65:10** Kum 32:2; 2Sam 1:21; Ay 36:28; Mdo 14:17
[k]**65:11** Kum 28:12; Za 104:3, 28; 147:14; Yn 10:10; Lk 6:38
[l]**65:12** Ay 28:26; Yoe 2:22; Za 98:8
[m]**65:13** Za 72:16; 98:8; 144:13; Zek 8:12; Isa 55:12; 44:23; 49:13; 30:33; 14:8
[n]**66:1** Za 81:1; 84:8; 98:4; 100:1
[o]**66:2** Za 79:9; 86:9; Isa 42:8, 12; 43:21
[p]**66:3** Kum 7:21; 10:21; Za 106:22; 111:6; 18:44; 65:5; 145:6; 2Sam 22:45
[q]**66:4** Za 22:27; 7:17; 67:3

5 [a]Njooni mwone yale Mungu
aliyoyatenda,
mambo ya kutisha aliyoyatenda
miongoni mwa wanadamu!
6 [b]Alifanya bahari kuwa nchi kavu,
wakapita kati ya maji kwa miguu,
njooni, tumshangilie.
7 [c]Yeye hutawala kwa uwezo wake
milele,
macho yake huangalia mataifa
yote:
waasi wasithubutu kujiinua dhidi
yake.

8 [d]Enyi mataifa, msifuni Mungu wetu,
sauti ya sifa yake isikike,
9 [e]ameyahifadhi maisha yetu
na kuizuia miguu yetu kuteleza.
10 [f]Ee Mungu, wewe ulitujaribu,
ukatusafisha kama fedha.
11 [g]Umetuingiza kwenye nyavu
na umetubebesha mizigo mizito
migongoni mwetu.
12 [h]Uliwaruhusu watu watukalie
vichwani,
tulipita kwenye moto na kwenye
maji,
lakini ulituleta kwenye nchi
iliyojaa utajiri tele.

13 [i]Nitakuja hekaluni mwako na sadaka
za kuteketezwa
na kukutimizia nadhiri zangu:
14 nadhiri ambazo midomo yangu
iliahidi
na nilizotamka kwa kinywa
changu
nilipokuwa katika shida.

15 [j]Nitakutolea dhabihu za wanyama
wanono
na sadaka za kondoo dume,
nitakutolea mafahali na mbuzi.

16 [k]Njooni msikilize ninyi nyote
mnaomcha Mungu,
nami niwaambie aliyonitendea.
17 Nilimlilia kwa kinywa changu,
sifa zake zilikuwa katika ulimi
wangu.
18 [l]Kama ningekuwa nimeyaficha
maovu moyoni mwangu,
Bwana asingekuwa amenisikiliza;
19 [m]lakini hakika Mungu amenisikiliza
na amesikia sauti yangu katika
maombi.
20 [n]Sifa apewe Mungu,
ambaye hakulikataa ombi langu
wala kunizuilia upendo wake!

## Zaburi 67

*Mataifa Yahimizwa Kumsifu Mungu*

*Kwa mwimbishaji. Na ala za nyuzi za muziki. Zaburi. Wimbo.*

1 [o]Mungu aturehemu na kutubariki,
na kutuangazia nuru za uso wake,
2 [p]ili njia zako zijulikane duniani,
wokovu wako katikati ya mataifa
yote.

3 [q]Ee Mungu, mataifa na wakusifu,
mataifa yote na wakusifu.
4 [r]Mataifa yote wafurahi na kuimba
kwa shangwe,
kwa kuwa unatawala watu kwa
haki
na kuongoza mataifa ya dunia.

---

[a]**66:5** Za 66:3; 46:8; 106:22
[b]**66:6** Mwa 8:1; Kut 14:21, 22; Law 23:40; Yos 3:14; Za 78:13; Isa 63:13, 14; 1Kor 10:1
[c]**66:7** Kut 15:18; 3:16; Hes 17:10; Za 11:4; 112:10; 140:8; 145:13
[d]**66:8** Za 22:23
[e]**66:9** Za 30:3; Kum 32:35; Ay 12:5
[f]**66:10** Kut 15:25; Ay 6:29; 28:1; Za 12:6; Zek 13:9
[g]**66:11** Za 38:4; 142:7; 146:7; Isa 61:1; 10:27; 42:7, 22; Mwa 3:17; Kut 1:14
[h]**66:12** Isa 51:13; Za 18:19
[i]**66:13** Za 51:19; 22:25; 50:14; 116:14; Mhu 5:4; Yon 2:9
[j]**66:15** Law 16:5; Za 51:19
[k]**66:16** Za 34:11; 71:15, 24
[l]**66:18** Kum 1:45; 1Sam 8:18; Yak 4:3; Isa 1:15; Ay 11:14, 15; Mit 15:29
[m]**66:19** Za 18:6
[n]**66:20** Za 22:24
[o]**67:1** Hes 6:24-26; Za 4:6; 31:16; 119:135; 2Kor 4:6
[p]**67:2** Isa 40:5; 52:10; 62:1, 2; Lk 2:30-32; Tit 2:11; Za 98:2; Mdo 10:35; 13:10
[q]**67:3** Za 67:5; Isa 24:15, 16
[r]**67:4** Za 100:1-2; 9:4; 96:10-13; 68:32

5 [a]Ee Mungu, mataifa na wakusifu,
mataifa yote na wakusifu.

6 [b]Ndipo nchi itatoa mazao yake,
naye Mungu, Mungu wetu,
atatubariki.
7 [c]Mungu atatubariki
na miisho yote ya dunia itamcha
yeye.

### Zaburi 68

*Wimbo Wa Taifa Wa Shangwe Kwa Ushindi*

*Kwa mwimbishaji. Zaburi ya Daudi. Wimbo.*

1 [d]Mungu na ainuke, watesi wake
watawanyike,
adui zake na wakimbie mbele
zake.
2 [e]Kama vile moshi upeperushwavyo
na upepo,
vivyo hivyo uwapeperushe mbali,
kama vile nta iyeyukavyo kwenye
moto,
vivyo hivyo waovu na waangamie
mbele za Mungu.
3 [f]Bali wenye haki na wafurahi,
washangilie mbele za Mungu,
wafurahi na kushangilia.

4 [g]Mwimbieni Mungu, liimbieni sifa
jina lake,
mtukuzeni yeye aendeshwaye juu
ya mawingu:
jina lake ni Bwana,
furahini mbele zake.
5 [h]Baba wa yatima, mtetezi wa wajane,
ni Mungu katika makao yake
matakatifu.
6 [i]Mungu huwaweka wapweke katika
jamaa,
huwaongoza wafungwa wakiimba,
bali waasi huishi katika nchi
kame.

7 [j]Ee Mungu, ulipowatangulia watu
wako,
ulipopita nyikani,
8 [k]dunia ilitikisika,
mbingu zikanyesha mvua,
mbele za Mungu, Yule wa Sinai,
mbele za Mungu, Mungu wa
Israeli.
9 [l]Ee Mungu, ulinyesha mvua nyingi
na kuiburudisha ardhi iliyokuwa
imechoka.
10 [m]Ee Mungu, watu wako waliishi
huko,
nawe kwa wingi wa utajiri wako
uliwapa maskini mahitaji yao.

11 [n]Bwana alitangaza neno,
waliolitangaza neno hilo walikuwa
kundi kubwa:
12 [o]"Wafalme na majeshi walikimbia
upesi,
watu waliobaki kambini
waligawana nyara.
13 [p]Hata ulalapo katikati ya mioto ya
kambini,
mabawa ya njiwa wangu
yamefunikwa kwa fedha,
manyoya yake kwa dhahabu
ing'aayo."
14 [q]Wakati Mwenyezi[r] alipowatawanya
wafalme katika nchi,
ilikuwa kama theluji iliyoanguka
juu ya Salmoni.

---

[a]**67:5** Za 67:3
[b]**67:6** Mwa 8:22; 12:2; Law 26:4; Za 85:12; Isa 55:10; Eze 34:27; Zek 8:12
[c]**67:7** Za 2:8; 33:8
[d]**68:1** Za 89:10; 132:8; 12:5; 18:14; 92:9; 144:6; Hes 10:35; Isa 17:13; 21:15; 33:3
[e]**68:2** Za 37:20; 80:16; 22:14; 9:3; Hes 10:35
[f]**68:3** Za 64:10; 97:12
[g]**68:4** 2Sam 22:50; Za 7:17; 30:4; 66:2; 68:33; 96:2; 100:4; 135:3; 83:18; Kut 6:3; 20:21; Kum 33:26
[h]**68:5** Za 10:14; Kut 22:22; Kum 10:18; 26:15; Yer 25:30
[i]**68:6** Lk 4:18; Za 146:7; 113:9; 102:20; 79:11; 25:16; Isa 58:11; 35:7; 49:10; 61:1
[j]**68:7** Kut 13:21; Za 78:40; 106:14
[k]**68:8** 2Sam 22:8; Amu 5:4, 5; Mhu 11:3; 2Sam 21:10; Kum 33:2
[l]**68:9** Kum 32:2; Ay 36:28; Eze 34:26
[m]**68:10** Kum 28:12; Za 65:9
[n]**68:11** Lk 2:13
[o]**68:12** Yos 10:16; Amu 5:30
[p]**68:13** Mwa 49:14
[q]**68:14** 2Sam 22:15; Amu 9:48
[r]14 Mwenyezi hapa ina maana ya Shaddai kwa Kiebrania.

15 Milima ya Bashani ni milima
iliyotukuka,
milima ya Bashani ina vilele
vilivyochongoka.
16 [a]Enyi milima yenye vilele
vilivyochongoka,
kwa nini mnakazia macho kwa
wivu,
katika mlima Mungu anaochagua
kutawala,
ambako BWANA mwenyewe
ataishi milele?
17 [b]Magari ya Mungu ni makumi ya
maelfu,
na maelfu ya maelfu;
Bwana amekuja kutoka Sinai
hadi katika patakatifu pake.
18 [c]Ulipopanda juu, uliteka mateka,
ukapokea vipawa kutoka kwa
wanadamu,
hata kutoka kwa wale walioasi,
ili wewe, Ee BWANA Mungu, upate
kuishi huko.

19 [d]Sifa apewe Bwana, Mungu Mwokozi
wetu,
ambaye siku kwa siku
hutuchukulia mizigo yetu.
20 [e]Mungu wetu ni Mungu aokoaye,
BWANA Mwenyezi hutuokoa na
kifo.

21 [f]Hakika Mungu ataponda vichwa vya
adui zake,
vichwa vya hao waendao katika
njia za dhambi.
22 [g]Bwana alisema, "Nitawarudisha
kutoka Bashani;
nitawarudisha kutoka vilindi vya
bahari,
23 [h]ili uweze kuchovya miguu yako
katika damu ya adui zako,
huku ndimi za mbwa wako zikiwa
na fungu lake."

24 [i]Ee Mungu, maandamano yako
yameonekana,
maandamano ya Mungu wangu,
Mfalme wangu,
yakielekea patakatifu pake.
25 [j]Mbele wako waimbaji, baada yao
wapiga vinanda,
pamoja nao wako wanawali
wakipiga matari.
26 [k]Msifuni Mungu katika kusanyiko
kubwa,
msifuni BWANA katika kusanyiko
la Israeli.
27 [l]Liko kabila dogo la Benyamini
likiwaongoza,
wakifuatwa na kundi kubwa la
watawala wa Yuda,
hatimaye watawala wa Zabuloni
na Naftali.

28 [m]Ee Mungu, amuru uwezo wako,
Ee Mungu tuonyeshe nguvu zako,
kama ulivyofanya hapo awali.
29 [n]Kwa sababu ya Hekalu lako
Yerusalemu
wafalme watakuletea zawadi.
30 [o]Mkemee mnyama aliyeko kwenye
manyasi,
kundi la mafahali katikati ya
ndama za mataifa.
Na walete minara ya madini ya
fedha wakinyenyekea.
Tawanya mataifa yapendayo vita.

---

[a]**68:16** Za 132:13, 14; 2:6; Kum 12:5
[b]**68:17** 2Fal 2:11; Isa 66:15; Hab 3:8; Dan 7:10
[c]**68:18** Za 47:5; 7:7; Amu 5:12; Efe 4:8; Hes 17:10
[d]**68:19** Za 65:5; 81:6
[e]**68:20** 1Sam 10:19; Za 56:13; Yer 45; 5; Eze 6:8
[f]**68:21** Za 74:14; 110:5; Hab 3:13
[g]**68:22** Ay 36:30; Mt 18:6
[h]**68:23** Za 58:10; 1Fal 21:19; 2Fal 9:36
[i]**68:24** Za 63:2
[j]**68:25** 1Nya 15:16; 6:31; 2Nya 5:12; Ufu 18:22; Mwa 31:27; Isa 5:12
[k]**68:26** Za 22:22; Ebr 2:12; Law 19:2
[l]**68:27** 1Sam 9:21; Hes 34:21; Amu 5:18
[m]**68:28** Kut 9:16; Za 29:11; Isa 26:12; 29:23; 45:11; 60:21; 64:8
[n]**68:29** 2Nya 9:24; 32:23
[o]**68:30** Isa 27:1; 34:7; 51:9; Ay 40:21; Eze 29:3; Za 22:12; 18:14; 120:7; 89:10; 140:2; Yer 50:27

31 [a]Wajumbe watakuja kutoka Misri,
Kushi[b] atajisalimisha kwa Mungu.

32 [c]Mwimbieni Mungu, enyi falme za dunia,
mwimbieni Bwana sifa,
33 [d]mwimbieni sifa yeye apandaye mbingu za kale zilizo juu,
yeye angurumaye kwa sauti kuu.
34 [e]Tangazeni uwezo wa Mungu,
ambaye fahari yake iko juu ya Israeli,
ambaye uwezo wake uko katika anga.
35 [f]Ee Mungu, wewe unatisha katika mahali patakatifu pako,
Mungu wa Israeli huwapa watu wake uwezo na nguvu.

Mungu Asifiwe!

## Zaburi 69

*Kilio Cha Kuomba Msaada Wakati Wa Dhiki*

*Kwa mwimbishaji. Mtindo wa "Yungiyungi." Zaburi ya Daudi.*

1 [g]Ee Mungu, niokoe,
kwa maana maji yamenifika shingoni.
2 [h]Ninazama kwenye vilindi vya matope,
pasipo mahali pa kukanyaga,
Nimefika kwenye maji makuu,
mafuriko yamenigharikisha.
3 [i]Nimechoka kwa kuomba msaada,
koo langu limekauka.
Macho yangu yanafifia,
nikimtafuta Mungu wangu.
4 [j]Wale wanaonichukia bila sababu
ni wengi kuliko nywele za kichwa changu;
wengi ni adui kwangu bila sababu,
wale wanaotafuta kuniangamiza.
Ninalazimishwa kurudisha
kitu ambacho sikuiba.

5 [k]Ee Mungu, wewe unajua upumbavu wangu,
wala hatia yangu haikufichika kwako.

6 Ee Bwana, ewe BWANA Mwenye Nguvu Zote,
wakutumainio wasiaibishwe
kwa ajili yangu;
wakutafutao wasifedheheshwe kwa ajili yangu,
Ee Mungu wa Israeli.
7 [l]Kwa maana nimestahimili dharau kwa ajili yako,
aibu imefunika uso wangu.
8 [m]Nimekuwa mgeni kwa ndugu zangu,
mgeni kwa wana wa mama yangu mwenyewe.
9 [n]Kwa kuwa wivu wa nyumba yako unanila,
matukano ya wale wanaokutukana yameniangukia.
10 [o]Ninapolia na kufunga,
lazima nivumilie matusi.
11 [p]Ninapovaa nguo ya gunia,
watu hunidharau.
12 [q]Wale wanaoketi mlangoni wananisimanga,
nimekuwa wimbo wa walevi.

13 [r]Lakini Ee BWANA, ninakuomba,
kwa wakati ukupendezao;

[a]**68:31** Isa 19:19; 43:3; 45:14; 11:11; 18:1; Sef 3:10
[b]31 Kushi hapa ina maana maeneo ya Naili ya juu, yaani Ethiopia.
[c]**68:32** Za 46:6; 67:4; 7:17
[d]**68:33** Kum 33:26; Kut 9:23; Za 29:3, 4; Isa 30:30; 33:3; 66:6; 45:3
[e]**68:34** Za 68:28; 45:3
[f]**68:35** Mwa 28:17; Isa 40:29; 41:10; 50:2; Za 66:20; 18:1; 29:11; 28:6; 2Kor 1:3; Kum 7:21
[g]**69:1** Za 42:7; 32:6; Yon 2:5
[h]**69:2** Ay 30:19
[i]**69:3** Za 6:6; 119:82
[j]**69:4** Yn 15:25; Za 25:19; 35:19; 38:19; 40:14; 119:95; Isa 32:7
[k]**69:5** Za 38:5; 44:21
[l]**69:7** Yer 15:15; Za 39:8; 44:15
[m]**69:8** Ay 19:13-15; Za 31:11; 38:11; Isa 53:3; Yn 7:5
[n]**69:9** Yn 2:17; Rum 15:3; Za 89:50-51
[o]**69:10** Za 35:13
[p]**69:11** 2Sam 3:31; Za 35:13
[q]**69:12** Mwa 18:1; 23:10; Ay 30:9
[r]**69:13** Isa 49:8; 2Kor 6:2; Za 17:7; 51:1

katika upendo wako mkuu, Ee Mungu,
unijibu kwa wokovu wako wa hakika.
14 [a]Uniokoe katika matope,
usiniache nizame;
niokoe na hao wanichukiao,
kutoka kwenye vilindi vya maji.
15 [bc]Usiache mafuriko yanigharikishe
au vilindi vinimeze,
au shimo lifumbe kinywa chake juu yangu.
16 [d]Ee BWANA, unijibu, kwa wema wa upendo wako;
kwa huruma zako nyingi unigeukie.
17 [e]Usimfiche mtumishi wako uso wako,
uharakishe kunijibu, kwa sababu niko katika shida.
18 [f]Njoo karibu uniokoe,
nikomboe kwa sababu ya adui zangu.

19 [g]Unajua jinsi ninavyodharauliwa,
kufedheheshwa na kuaibishwa,
adui zangu wote unawajua.
20 [h]Dharau zimenivunja moyo
na nimekata tamaa,
nimetafuta wa kunihurumia, lakini sikumpata,
wa kunituliza, lakini sikumpata.
21 [i]Waliweka nyongo katika chakula changu
na walinipa siki nilipokuwa na kiu.

22 [j]Meza iliyoandaliwa mbele yao na iwe mtego,
nayo iwe upatilizo na tanzi.
23 [k]Macho yao yatiwe giza ili wasiweze kuona,
nayo migongo yao iinamishwe daima.
24 [l]Uwamwagie ghadhabu yako,
hasira yako kali na iwapate.
25 [m]Mahali pao na pawe ukiwa,
wala asiwepo yeyote atakayeishi katika mahema yao.
26 [n]Kwa kuwa wanawatesa wale uliowajeruhi,
na kuzungumza juu ya maumivu ya wale uliowaumiza.
27 [o]Walipize uovu juu ya uovu,
usiwaache washiriki katika wokovu wako.
28 [p]Wafutwe kutoka kitabu cha uzima
na wasiorodheshwe pamoja na wenye haki.

29 [q]Mimi niko katika maumivu na dhiki;
Ee Mungu, wokovu wako na unihifadhi.

30 [r]Nitalisifu jina la Mungu kwa wimbo,
nami nitamtukuza kwa kumtolea shukrani.
31 [s]Hili litampendeza BWANA kuliko ng'ombe dume,
zaidi ya fahali akiwa na pembe na kwato zake.
32 [t]Maskini wataona na kufurahi:
ninyi mnaomtafuta Mungu, mioyo yenu na iishi!
33 [u]BWANA huwasikia wahitaji
wala hadharau watu wake waliotekwa.

[a]**69:14** Za 69:2; 144:7
[b]**69:15** Za 36:6; 68:22; Hes 21:33; Yer 22:20
[c]**69:15** Za 28:1; 124:4, 5; Hes 16:33
[d]**69:16** Za 63:3
[e]**69:17** Za 22:24; 143:7; 50:15; 66:14
[f]**69:18** Za 49:15
[g]**69:19** Za 22:6
[h]**69:20** Ay 16:2; Isa 63:5; Za 142:4
[i]**69:21** Hes 6:3; Lk 23:36; Mt 27:34, 48; Mk 15:23, 36; Yn 19:28-30
[j]**69:22** 1Sam 28:9; Ay 18:10
[k]**69:23** Rum 11:9-10
[l]**69:24** Za 79:6; Yer 10:25
[m]**69:25** Law 26:43; Mt 23:38; Mdo 1:20
[n]**69:26** Ay 19:22; Zek 1:15
[o]**69:27** Neh 4:5; Za 109:14
[p]**69:28** Kut 32:32-33; Lk 10:20; Eze 13:9
[q]**69:29** Za 20:1
[r]**69:30** Za 28:7; 34:3
[s]**69:31** Za 50:9-13; 51:16
[t]**69:32** Za 34:2; 22:26
[u]**69:33** Za 12:5

34 [a]Mbingu na dunia zimsifu,
bahari na vyote viendavyo ndani yake,
35 [b]kwa maana Mungu ataiokoa Sayuni
na kuijenga tena miji ya Yuda.
Kisha watu watafanya makao yao humo na kuimiliki,
36 [c]watoto wa watumishi wake watairithi
na wale wote walipendao jina lake wataishi humo.

### Zaburi 70

*Kuomba Msaada*

**(Zaburi 40:13-17)**

*Kwa mwimbishaji. Zaburi ya Daudi. Maombi.*

1 [d]Ee Mungu, ufanye haraka kuniokoa;
Ee BWANA, njoo hima unisaidie.
2 [e]Wale wanaotafuta kuuondoa uhai wangu,
waaibishwe na kufadhaishwa;
wote wanaotamani kuangamizwa kwangu,
warudishwe nyuma kwa aibu.
3 Wale waniambiao, “Aha! Aha!”
warudi nyuma kwa sababu ya aibu yao.
4 [f]Lakini wote wakutafutao
washangilie na kukufurahia,
wale wapendao wokovu wako siku zote waseme,
“Mungu na atukuzwe!”

5 [g]Lakini bado mimi ni maskini na mhitaji;
Ee Mungu, unijie haraka.
Wewe ndiwe msaada wangu na mwokozi wangu;
Ee BWANA, usikawie.

### Zaburi 71

*Kuomba Ulinzi Na Msaada Siku Zote Za Maisha*

1 [h]Ee BWANA, nimekukimbilia wewe,
usiache nikaaibika kamwe.
2 [ij]Kwa haki yako uniponye na kuniokoa,
unitegee sikio lako uniokoe.
3 [k]Uwe kwangu mwamba wa kimbilio,
mahali nitakapokimbilia kila wakati;
toa amri ya kuniokoa, kwa kuwa wewe
ni mwamba wangu na ngome yangu.
4 [l]Ee Mungu wangu uniokoe kutoka kwenye mkono wa mwovu,
kutoka kwenye makucha ya watu wabaya na wakatili.

5 [m]Kwa kuwa umekuwa tumaini langu, Ee BWANA Mwenyezi,
tegemeo langu tangu ujana wangu.
6 [n]Tangu kuzaliwa nimekutegemea wewe,
ulinitoa tumboni mwa mama yangu.
Nitakusifu wewe daima.
7 [o]Nimekuwa kama kioja kwa wengi,
lakini wewe ni kimbilio langu imara.
8 [p]Kinywa changu kimejazwa sifa zako,
nikitangaza utukufu wako mchana kutwa.

9 [q]Usinitupe wakati wa uzee,
wala usiniache nguvu zangu zinapopungua.

---

[a]**69:34** Za 96:11; 98:7; Isa 44:23
[b]**69:35** Oba 1:17; Ezr 9:9; Za 51:18
[c]**69:36** Za 25:13; 37:29
[d]**70:1** Za 35:4; 6:10; 35:26; 71:12; 109:29; 129:5
[e]**70:2** Za 35:2
[f]**70:4** Za 31:6, 7; 35:27; 32:11; 118:24; 9:10
[g]**70:5** Za 109:22; 141:1; 30:10; 86:1; 33:10; 18:2; 119:60
[h]**71:1** Kum 23:15; Rut 2:12; Za 22:5
[i]**71:2** 2Fal 19:16
[j]**71:2** Kut 34:6
[k]**71:3** Za 18:2
[l]**71:4** 2Fal 19:19; Za 140:4; Mwa 48:16
[m]**71:5** Za 9:18; 25:5; Ay 4:6; Yer 17:7
[n]**71:6** Ay 3:16; Za 9:1; 22:9; 34:1; 52:9; 119:164; 145:2
[o]**71:7** Kum 28:46; 1Kor 4:9; Za 61:3; 2Sam 22:3
[p]**71:8** Za 71:15; 51:15; 63:5; 96:6; 104:1
[q]**71:9** Za 51:11; 92:14; Kum 4:31; 31:6

10 [a]Kwa maana adui zangu
wananisengenya,
wale wanaonivizia kuniua
wafanya hila.
11 [b]Wanasema, “Mungu amemwacha,
mkimbilieni mkamkamate,
kwani hakuna wa kumwokoa.”
12 [c]Ee Mungu, usiwe mbali nami,
njoo haraka kunisaidia, Ee Mungu
wangu.
13 [d]Washtaki wangu na waangamie kwa
aibu,
wale wanaotaka kunidhuru
na wafunikwe kwa dharau na
fedheha.

14 [e]Lakini mimi, nitatumaini siku zote,
nitakusifu zaidi na zaidi.
15 [f]Kinywa changu kitasimulia haki
yako,
wokovu wako mchana kutwa,
ingawa sifahamu kipimo chake.
16 [g]Ee BWANA Mwenyezi, nitakuja
na kutangaza matendo yako
makuu,
nitatangaza haki yako, yako peke
yako.
17 [h]Ee Mungu, umenifundisha tangu
ujana wangu,
hadi leo ninatangaza matendo
yako ya ajabu.
18 [i]Ee Mungu, usiniache,
hata niwapo mzee wa mvi,
mpaka nitangaze uwezo wako kwa
kizazi kijacho,
nguvu zako kwa wote watakaokuja
baadaye.

19 [j]Ee Mungu, haki yako imefika juu
katika mbingu,
wewe ambaye umefanya mambo
makuu.
Ee Mungu, ni nani aliye kama
wewe?
20 [k]Ingawa umenifanya nipate taabu,
nyingi na chungu,
utanihuisha tena,
kutoka vilindi vya dunia
utaniinua tena.
21 [l]Utaongeza heshima yangu
na kunifariji tena.

22 [m]Ee Mungu wangu, nitakusifu kwa
kinubi
kwa ajili ya uaminifu wako;
Ee Uliye Mtakatifu wa Israeli,
nitakuimbia sifa kwa zeze.
23 [n]Midomo yangu itapaza sauti kwa
furaha
ninapokuimbia sifa,
mimi, ambaye umenikomboa.
24 [o]Ulimi wangu utasimulia matendo
yako ya haki
mchana kutwa,
kwa maana wale waliotaka
kunidhuru,
wameaibishwa na kufadhaishwa.

## Zaburi 72

*Maombi Kwa Ajili Ya Mfalme*

*Zaburi ya Solomoni.*

1 [p]Ee Mungu, mjalie mfalme aamue
kwa haki yako,
mwana wa mfalme kwa haki yako.
2 [q]Atawaamua watu wako kwa haki,
watu wako walioonewa kwa haki.
3 Milima italeta mafanikio kwa watu,
vilima tunda la haki.

[a]**71:10** Za 3:7; 10:8; 59:3; 31:13; Mt 1:10; 12:14
[b]**71:11** Isa 40:27; 54:7; Mt 27:46; Za 7:2; 9:10; Mao 5:20
[c]**71:12** Za 38:21, 22; 22:19
[d]**71:13** Ay 8:22; Za 15:3; 70:2; Yer 18:19
[e]**71:14** Za 25:3; 42:5; 130:7; 131:3
[f]**71:15** Za 71:8; 66:6; 51:14
[g]**71:16** Za 77:12; 106:2; 118:15; 9:1; 145:4
[h]**71:17** Yer 7:13; Ay 5:9; Za 26:7; 86:10; 96:3; Kum 4:5
[i]**71:18** Isa 46:4; Kut 9:16; Ay 8:8; Yoe 1:3; Za 78:4; 145:4; 22:30, 31
[j]**71:19** Lk 1:49; Za 36:5; 35:10; 77:13; 89:8; 126:2
[k]**71:20** Za 80:3, 19; 25:17; 85:4; 63:9; Hos 6:2
[l]**71:21** Za 18:35; 86:17; Isa 12:1; 40:1, 2; 49:13; 54:10
[m]**71:22** Za 33:2; 92:3; 144:9; Ay 21:12; 2Fal 19:22
[n]**71:23** Za 20:5; Kut 15:13
[o]**71:24** Za 35:28; Es 9:2
[p]**72:1** Kum 1:16; Za 9:8
[q]**72:2** Isa 11:2, 4, 5; 16:5; 9:7; Yer 23:5; 33:15

4 [a]Atawatetea walioonewa miongoni
mwa watu
na atawaokoa watoto wa wahitaji,
ataponda mdhalimu.

5 [b]Atadumu kama jua lidumuvyo,
kama mwezi, vizazi vyote.
6 [c]Atakuwa kama mvua inyeshayo juu
ya shamba lililofyekwa,
kama manyunyu yanyeshayo
ardhi.
7 [d]Katika siku zake wenye haki
watastawi;
mafanikio yatakuwepo mpaka
mwezi utakapokoma.

8 [e]Atatawala kutoka bahari hadi
bahari
na kutoka Mto[f] mpaka miisho ya
dunia.
9 Makabila ya jangwani watamsujudia,
na adui zake wataramba
mavumbi.
10 [g]Wafalme wa Tarshishi na wa pwani
za mbali
watamletea kodi;
wafalme wa Sheba na Seba
watampa zawadi.
11 [h]Wafalme wote watamsujudia
na mataifa yote yatamtumikia.

12 Kwa maana atamwokoa mhitaji
anayemlilia,
aliyeonewa asiye na wa
kumsaidia.
13 [i]Atawahurumia wanyonge na
wahitaji
na kuwaokoa wahitaji kutoka
mauti.
14 [j]Atawaokoa kutoka uonevu na
ukatili,
kwani damu yao ni ya thamani
machoni pake.

15 [k]Aishi maisha marefu!
Na apewe dhahabu ya Sheba.
Watu wamwombee daima
na kumbariki mchana kutwa.
16 [l]Nafaka ijae tele katika nchi yote,
juu ya vilele vya vilima na istawi.
Tunda lake na listawi kama
Lebanoni,
listawi kama majani ya kondeni.
17 [m]Jina lake na lidumu milele,
na lidumu kama jua.

Mataifa yote yatabarikiwa kupitia
kwake,
nao watamwita aliyebarikiwa.

18 [n]BWANA Mungu, Mungu wa Israeli,
apewe sifa,
yeye ambaye peke yake hutenda
mambo ya ajabu.
19 [o]Jina lake tukufu lisifiwe milele,
ulimwengu wote ujae utukufu
wake.
Amen na Amen.

---

[a]**72:4** Za 27:11; 76:9; 9:12; Isa 49:13; 11:4; 29:19; 32:7
[b]**72:5** 1Sam 13:13; Za 33:11
[c]**72:6** Kum 32:2
[d]**72:7** Za 92:12; Mit 14:11
[e]**72:8** Kut 23:31; 1Fal 4:21; Zek 9:10
[f]8 Yaani Mto Frati.
[g]**72:10** Mwa 10:4, 7; Es 10:1; 1Fal 9:16; 2Nya 9:24
[h]**72:11** Mwa 27:29; Ezr 1:2
[i]**72:13** Isa 60:10; Yoe 2:18; Lk 10:33
[j]**72:14** Za 69:18; Eze 13:23; 34:10; 1Sam 26:21
[k]**72:15** Mwa 10:7; Za 35:28
[l]**72:16** Eze 34:27; Isa 4:2; 27:6; 44:4; 58:11; 66:14; Mwa 27:18; Hes 22:4; Za 4:7; 92:12; 104:16
[m]**72:17** Kut 3:15; Lk 1:48; Za 89:36; Mwa 12:3
[n]**72:18** 1Nya 29:10; Za 41:13; 106:48; Lk 1:68; Ay 5:9
[o]**72:19** 2Sam 7:26; Hes 14:21; Za 41:13

[20] [a]Huu ndio mwisho wa maombi ya
Daudi mwana wa Yese.

## KITABU CHA TATU

*(Zaburi 73–89)*

### Zaburi 73

*Haki Ya Mungu*

*Zaburi ya Asafu.*

[1] [b]Hakika Mungu ni mwema kwa
Israeli,
kwa wale ambao mioyo yao ni
safi.

[2] [c]Bali kwangu mimi, miguu yangu
ilikuwa karibu kuteleza;
nilikuwa karibu mguu wangu
kuachia uliposimama.
[3] [d]Kwa maana niliwaonea wivu wenye
kujivuna
nilipoona kufanikiwa kwa waovu.

[4] Wao hawana taabu,[e]
miili yao ina afya na nguvu.
[5] [f]Hawapati shida zinazowataabisha
watu wengine,
wala hawapati mapigo kama
wanadamu wengine.
[6] [g]Kwa hiyo kiburi ni mkufu wao,
wamejivika jeuri.
[7] [h]Uovu hutoka katika mioyo yao
iliyokufa ganzi,
majivuno maovu kutoka mioyoni
mwao hauna kikomo.
[8] [i]Hudhihaki na kusema kwa ukorofi,
katika majivuno yao wanatishia
kutesa.
[9] [j]Vinywa vyao huweka madai hata
kwa mbingu,
nazo ndimi zao humiliki duniani.
[10] Kwa hiyo watu wao huwageukia
na kunywa maji tele.[k]
[11] [l]Wanasema, "Mungu awezaje kujua?
Je, Yeye Aliye Juu Sana anayo
maarifa?"

[12] [m]Hivi ndivyo walivyo waovu:
siku zote hawajali,
wanaongezeka katika utajiri.

[13] [n]Hakika nimeuweka moyo wangu
safi bure,
ni bure nimenawa mikono yangu
nisiwe na hatia.
[14] [o]Mchana kutwa nimetaabika,
nimeadhibiwa kila asubuhi.

[15] Kama ningesema, "Nitasema hivi,"
ningelikuwa nimewasaliti watoto
wako.
[16] [p]Nilipojaribu kuelewa haya yote,
yalikuwa magumu kwangu
kuelewa.
[17] [q]Mpaka nilipoingia patakatifu pa
Mungu,
ndipo nilipotambua mwisho wao.

[18] [r]Hakika unawaweka mahali pa
utelezi,
unawaangusha chini kwa
uharibifu.
[19] [s]Tazama jinsi wanavyoangamizwa
ghafula,
wanatoweshwa kabisa na vitisho!

---

[a]**72:20** Rut 4:17
[b]**73:1** Za 24:4; 5:8
[c]**73:2** Kum 32:35; Za 69:2; Efe 4:27
[d]**73:3** Mit 3:31; 23:17; 24:1-2; Ay 9:24; 21:7; Yer 12:1; Mal 3:15
[e]4 Tafsiri nyingine zinasema: hawana maumivu katika kufa kwao.
[f]**73:5** Za 73:12; Eze 23:42
[g]**73:6** Law 26:19; Mwa 6:11; 41:42; Wim 4:9; Eze 16:11; Mit 4:17; Mhu 8:11
[h]**73:7** Za 7:10
[i]**73:8** Za 10:7; 12:5; 41:5; Eze 25:15; Kol 3:8; 2Pet 2:18; Yud 16
[j]**73:9** Ufu 13:6
[k]10 Au: na kupokea yote wasemayo.
[l]**73:11** Ay 22:13; Za 94:7
[m]**73:12** Za 73:5; 49:6
[n]**73:13** Ay 9:29-31; 21:15; Za 24:4; Mal 3:14; Mwa 44:16; Ebr 10:19-22
[o]**73:14** Za 73:5
[p]**73:16** Mhu 8:17
[q]**73:17** Kut 15:17; Ay 8:13; Flp 3:19; Za 15:1; 77:13
[r]**73:18** Kum 32:35; Za 35:6; 17:13
[s]**73:19** Kum 28:20; Mit 24:22; Isa 47:11; Mwa 19:15

[20] [a]Kama ndoto mtu aamkapo,
hivyo wakati uinukapo, Ee BWANA,
utawatowesha kama ndoto.

[21] Wakati moyo wangu ulipohuzunishwa,
na roho yangu ilipotiwa uchungu,
[22] [b]nilikuwa mpumbavu na mjinga,
nilikuwa mnyama mkatili mbele yako.

[23] [c]Hata hivyo niko pamoja nawe siku zote,
umenishika mkono wangu wa kuume.
[24] [d]Unaniongoza kwa shauri lako,
hatimaye utaniingiza katika utukufu.
[25] [e]Nani niliye naye mbinguni ila wewe?
Dunia haina chochote ninachokitamani ila wewe.
[26] [f]Mwili na moyo wangu vyaweza kushindwa,
bali Mungu ni nguvu ya moyo wangu
na fungu langu milele.

[27] [g]Wale walio mbali nawe wataangamia,
unawaangamiza wote wasio waaminifu kwako.
[28] [h]Lakini kwangu mimi,
ni vyema kuwa karibu na Mungu.
Nimemfanya BWANA Mwenyezi kimbilio langu;
nami nitayasimulia matendo yako yote.

[a]**73:20** Za 78:65; Isa 29:8; Ay 20:8; Mit 12:11; 28:19
[b]**73:22** Za 49:10; 92:6; 49:12, 20; Mhu 3:18; 9:12
[c]**73:23** Mwa 48:13
[d]**73:24** Za 48:14; 1Fal 22:5; Isa 58:8; Yn 14:3; 2Kor 5:1
[e]**73:25** Za 16:2; Flp 3:8
[f]**73:26** Kum 32:9; Za 18:1; 84:2; 31:10; 40:12
[g]**73:27** Za 34:21; Law 6:2; Yer 5:11; Hos 4:12; 9:1
[h]**73:28** Sef 3:2; Yak 4:8; Za 40:5; 26:7; 9:9; Ebr 10:22

## Zaburi 74

*Maombi Kwa Ajili Ya Taifa Kuokolewa*

*Utenzi wa Asafu.*

[1] [i]Ee Mungu, mbona umetukataa milele?
Mbona hasira yako inatoka moshi
juu ya kondoo wa malisho yako?
[2] [j]Kumbuka watu uliowanunua zamani,
kabila la urithi wako, ambao uliwakomboa:
Mlima Sayuni, ambamo uliishi.
[3] [k]Geuza hatua zako kuelekea magofu haya ya kudumu,
uharibifu wote huu ambao adui ameuleta pale patakatifu.

[4] [l]Adui zako wamenguruma pale ulipokutana nasi,
wanaweka bendera zao kama alama.
[5] [m]Walifanya kama watu wanaotumia mashoka
kukata kichaka cha miti.
[6] [n]Walivunjavunja milango yote iliyonakshiwa
kwa mashoka na vishoka vyao.
[7] [o]Waliteketeza kabisa mahali pako patakatifu,
wakayanajisi makao ya Jina lako.
[8] [p]Walisema mioyoni mwao,
"Tutawaponda kabisa!"
Walichoma kila mahali ambapo Mungu
aliabudiwa katika nchi.
[9] [q]Hatukupewa ishara za miujiza;
hakuna manabii waliobaki,

[i]**74:1** Yer 23:1; Za 43:2; 44:23; 95:7; 79:13; 100:3; Eze 34:8, 31; Lk 12:32
[j]**74:2** 1Kor 6:20; Kum 32:7; Kut 34:9; 15:13, 16; Isa 48:20; Za 2:6; 43:3; 68:16; Isa 46:13; Oba 1:17; Yoe 3:17, 21
[k]**74:3** Isa 44:26; 52:9
[l]**74:4** Mao 2:7; Hes 2:2; Yer 4:6; Dan 6:27
[m]**74:5** Yer 46:23
[n]**74:6** 1Fal 6:18
[o]**74:7** Law 15:31; 20:3; Mdo 21:28; Za 75:1
[p]**74:8** 2Fal 25:9; Za 83:4; 94:5; Yer 34:22; 52:13; 21:10; 2Nya 36:19
[q]**74:9** Kut 4:17; 10:1; 1Sam 3:1; Mik 3:6; Mt 16:4

hakuna yeyote kati yetu ajuaye
hali hii itachukua muda gani.

10 [a]Ee Mungu, mtesi atakudhihaki mpaka lini?
Je, adui watalitukana jina lako milele?
11 [b]Kwa nini unazuia mkono wako,
mkono wako wa kuume?
Uutoe kutoka makunjo ya vazi lako
na uwaangamize!

12 [c]Lakini wewe, Ee Mungu, ni mfalme wangu tangu zamani,
unaleta wokovu duniani.
13 [d]Ni wewe uliyeigawanya bahari kwa uweza wako;
ulivunja vichwa vya wanyama wakubwa wa kutisha katika maji.
14 [e]Ni wewe uliyeponda vichwa vya Lewiathani[f]
nawe ukamtoa kama chakula
kwa viumbe vya jangwani.
15 [g]Ni wewe uliyefungua chemchemi na vijito,
ulikausha mito ambayo ilikuwa ikitiririka daima.
16 [h]Mchana ni wako, nao usiku ni wako pia,
uliziweka jua na mwezi.
17 [i]Ni wewe uliyeiweka mipaka yote ya dunia,
ulifanya kiangazi na masika.

18 [j]Ee BWANA, kumbuka jinsi mtesi alivyokudhihaki,
jinsi watu wapumbavu walivyolitukana jina lako.
19 [k]Usiukabidhi uhai wa njiwa wako kwa wanyama wakali wa mwitu;
usisahau kabisa uhai wa watu wako wanaoteseka milele.
20 [l]Likumbuke agano lako,
maana mara kwa mara mambo ya jeuri
yamejaa katika sehemu za giza nchini.
21 [m]Usiruhusu walioonewa warudi nyuma kwa aibu;
maskini na wahitaji hebu walisifu jina lako.

22 [n]Inuka, Ee Mungu, ujitetee;
kumbuka jinsi wapumbavu
wanavyokudhihaki mchana kutwa.
23 [o]Usipuuze makelele ya watesi wako,
ghasia za adui zako, zinazoinuka mfululizo.

## Zaburi 75

*Mungu Ni Mwamuzi*

*Kwa mwimbishaji. Mtindo wa "Usiharibu!" Zaburi ya Asafu. Wimbo.*

1 [p]Ee Mungu, tunakushukuru,
tunakushukuru wewe,
kwa kuwa jina lako li karibu;
watu husimulia matendo yako ya ajabu.

2 [q]Unasema, "Ninachagua wakati maalum;
ni mimi nihukumuye kwa haki.

---

[a]**74:10** Za 6:3; 79:5; 80:4; 74:22; 44:16
[b]**74:11** Kut 15:6; Neh 5:13; Eze 5:3
[c]**74:12** Za 2:6; 24:7; 68:24; 44:4
[d]**74:13** Isa 51:9; 27:1; Eze 29:3; 32:2; Kut 14:21
[e]**74:14** Hes 14:9; Za 72:9; Ay 3:8; Isa 13:21; 23:13; 34:14; Yer 50:39
[f]14 Lewiathani ni mnyama mkubwa wa baharini mwenye magamba anayefanana na joka kubwa, mwenye umbo la kutisha, asiyeweza kuvuliwa.
[g]**74:15** Kut 14:29; 17:6; Hes 20:11; Isa 11:16; Hab 3:9; Ufu 16:12; Yos 2:10
[h]**74:16** Mwa 1:16; Za 136:7-9
[i]**74:17** Mdo 17:26; Kum 32:8; Mwa 8:22
[j]**74:18** Ufu 16:19; Kum 32:9
[k]**74:19** Mwa 8:8; Isa 59:11; Za 9:18
[l]**74:20** Mwa 6:18; 17:7; Law 26:44; Yer 33:21; Ay 34:22
[m]**74:21** Isa 58:10; Za 9:9, 18; 10:18; 103:6; 35:10
[n]**74:22** Za 17:13; 53:1
[o]**74:23** Isa 31:4; Za 65:7; 46:6; Hes 25:17
[p]**75:1** Yos 3:5; Za 44:1; 71:16; 77:12; 105:2; 107:8, 15; 145:5, 12, 18
[q]**75:2** Kut 13:10; Za 7:11

3 [a]Wakati dunia na watu wake wote
inapotetemeka,
ni mimi ninayezishikilia nguzo
zake imara.
4 [b]Kwa wale wenye majivuno
ninasema,
'Msijisifu tena,'
kwa wale waovu, 'Msiinue pembe
zenu.
5 [c]Msiinue pembe zenu dhidi ya
mbingu;
msiseme kwa shingo
zilizonyooshwa.' "

6 Hakuna yeyote atokaye mashariki
wala magharibi
au kutoka jangwani awezaye
kumkweza mwanadamu.
7 [d]Bali Mungu ndiye ahukumuye:
Humshusha huyu na kumkweza
mwingine.
8 [e]Mkononi mwa BWANA kuna
kikombe
kilichojaa mvinyo unaotoka povu
uliochanganywa na vikolezo;
huumimina, nao waovu wote wa
dunia
hunywa mpaka tone la mwisho.

9 [f]Bali mimi, nitatangaza hili milele;
nitaimba sifa kwa Mungu wa
Yakobo.
10 [g]Nitazikatilia mbali pembe za waovu
wote,
bali pembe za wenye haki
zitainuliwa juu.

## Zaburi 76

*Mungu Wa Israeli Ni Mhukumu Wa Dunia Yote*

*Kwa mwimbishaji. Kwa ala za nyuzi za muziki. Zaburi ya Asafu. Wimbo.*

1 [h]Katika Yuda, Mungu anajulikana,
jina lake ni kuu katika Israeli.
2 [i]Hema lake liko Salemu,
makao yake katika Sayuni.
3 [j]Huko alivunja mishale imetametayo,
ngao na panga, silaha za vita.

4 [k]Wewe unang'aa kwa mwanga,
mwenye fahari zaidi ya milima
yenye utajiri wa wanyama
pori.
5 [l]Mashujaa hulala wametekwa nyara,
hulala usingizi wao wa mwisho;
hakuna hata mmoja wa watu wa vita
anayeweza kuinua mikono yake.
6 [m]Kwa kukemea kwako, Ee Mungu wa
Yakobo,
farasi na gari la vita vilikaa kimya.
7 [n]Wewe peke yako ndiye wa
kuogopwa.
Ni nani awezaye kusimama mbele
yako unapokasirika?
8 [o]Kutoka mbinguni ulitamka hukumu,
nayo nchi ikaogopa, ikawa kimya:
9 [p]wakati wewe, Ee Mungu, ulipoinuka
kuhukumu,
kuwaokoa wote walioonewa
katika nchi.
10 [q]Hakika ghadhabu yako dhidi ya
wanadamu inakuletea sifa,
na masalia ya ghadhabu yako
unajifunga mshipi.

---

[a]**75:3** Ebr 1:3; Isa 24:19; 1Sam 2:8; 2Sam 22:8
[b]**75:4** Za 5:5; Zek 1:21; 1Sam 2:3
[c]**75:5** Ay 15:25
[d]**75:7** Mwa 16:5; Ufu 18:8; 1Sam 2:7; Ay 5:11; Za 50:6; 58:11; 147:6; Eze 21:26; Dan 2:21; Lk 1:52
[e]**75:8** Mit 23:30; Isa 51:17; Yer 25:15; Zek 12:2; Ufu 14:10; Ay 21:20
[f]**75:9** Za 40:10; 76:6; 108:1; Mwa 24:12
[g]**75:10** Za 89:17; 92:10; 112:9; 148:14

[h]**76:1** Za 99:3
[i]**76:2** Mwa 14:18; Ebr 7:1; Za 2:6; 2Sam 5:7
[j]**76:3** Za 46:9; Eze 39:9
[k]**76:4** Za 36:9; Eze 38:12
[l]**76:5** Amu 20:44; Za 13:3; Mt 9:24; Isa 46:12; Yer 51:39
[m]**76:6** Kut 15:1; Zek 12:4; Nah 2:13; Za 50:21
[n]**76:7** Ay 41:10; Nah 1:6; 1Nya 16:25; Ezr 9:15; Ufu 6:17; Za 2:5
[o]**76:8** 1Nya 16:30; Eze 38:20
[p]**76:9** Za 9:8; 58:11; 74:22; 82:8; 96:13; 72:4
[q]**76:10** Kut 9:16; Rum 9:17

11 [a]Wekeni nadhiri kwa BWANA Mungu
wenu na kuzitimiza;
nchi zote za jirani na walete
zawadi
kwa Yule astahiliye kuogopwa.
12 Huvunja roho za watawala;
anaogopwa na wafalme wa dunia.

### Zaburi 77

*Matendo Makuu Ya Mungu Yanakumbukwa*

*Kwa mwimbishaji. Mtindo wa Yeduthuni. Zaburi ya Asafu.*

1 [b]Nilimlilia Mungu ili anisaidie,
nilimlilia Mungu ili anisikie.
2 [c]Nilipokuwa katika taabu,
nilimtafuta Bwana,
usiku nilinyoosha mikono bila
kuchoka
na nafsi yangu ilikataa kufarijika.

3 [d]Ee Mungu, nilikukumbuka wewe,
nikalia kwa huzuni;
nikatafakari, roho yangu
ikadhoofika.
4 [e]Ulizuia macho yangu kufumba;
nilikuwa nasumbuka, nikashindwa
kusema.
5 [f]Nilitafakari juu ya siku zilizopita,
miaka mingi iliyopita,
6 nilikumbuka nilivyoimba nyimbo
usiku.
Moyo wangu ulitafakari
na roho yangu ikauliza:

7 [g]"Je, Bwana atakataa milele?
Je, hatatenda mema tena?
8 [h]Je, upendo wake usio na mwisho
umetoweka milele?
Je, ahadi yake imekoma nyakati
zote?
9 [i]Je, Mungu amesahau kuwa na
huruma?
Je, katika hasira amezuia huruma
yake?"

10 [j]Ndipo nikawaza, "Huu ndio udhaifu
wangu:
lakini nitakumbuka
miaka ya mkono wa kuume
wa Aliye Juu Sana."
11 [k]Nitayakumbuka matendo ya
BWANA;
naam, nitaikumbuka miujiza yako
ya zamani.
12 [l]Nitazitafakari kazi zako zote
na kuyawaza matendo yako
makuu.

13 [m]Ee Mungu, njia zako ni takatifu.
Ni mungu yupi aliye mkuu kama
Mungu wetu?
14 [n]Wewe ndiwe Mungu utendaye
miujiza,
umeonyesha uwezo wako katikati
ya mataifa.
15 [o]Kwa mkono wako wenye nguvu
umewakomboa watu wako,
uzao wa Yakobo na Yosefu.

16 [p]Maji yalikuona, Ee Mungu,
maji yalikuona yakakimbia,
vilindi vilitetemeka.

---

[a]**76:11** Mhu 5:4-5; Za 68:35; Law 22:18; Za 50:14; 2Nya 32:23
[b]**77:1** 1Fal 8:52
[c]**77:2** Mwa 37:35; 32:7; 2Sam 22:7; Za 118:5; 6:6; 22:2; 88:1; 50:15; Kut 9:29; Ay 11:13; Mt 2:18; Isa 26:9
[d]**77:3** Za 6:6; 78:35; Kut 2:23; Yer 45:3; 6:2
[e]**77:4** Za 39:2
[f]**77:5** Kum 32:7; Isa 51:9; Za 44:1; 143:5; Mhu 7:16
[g]**77:7** Za 85:1; 102:13; 106:4; 1Nya 28:9
[h]**77:8** Za 6:4; 90:14; 2Pet 3:9; Isa 27:11; Yn 2:4; Hes 23:19; Yer 15:18; Rum 9:6
[i]**77:9** Za 25:6; 40:11; 51:1; Isa 49:15
[j]**77:10** Ay 42:3; Za 31:22; Yer 10:19; Kut 15:6
[k]**77:11** Neh 9:17; 1Nya 16:12; Za 28:5; Isa 5:14
[l]**77:12** Mwa 24:63; Za 143:5
[m]**77:13** Za 73:17; 71:19; 86:8; Kut 15:11
[n]**77:14** Kut 3:20; 34:10
[o]**77:15** Kut 6:6
[p]**77:16** Kut 14:21, 28; Isa 50:2; Hab 3:8, 10; Yos 3:15, 16; Za 114:4

17 [a]Mawingu yalimwaga maji,
mbingu zikatoa ngurumo kwa radi,
mishale yako ikametameta huku na huko.
18 [b]Ngurumo yako ilisikika katika upepo wa kisulisuli,
umeme wako wa radi ukaangaza dunia,
nchi ikatetemeka na kutikisika.
19 [c]Njia yako ilipita baharini,
mapito yako kwenye maji makuu,
ingawa nyayo zako hazikuonekana.

20 [d]Uliongoza watu wako kama kundi
kwa mkono wa Mose na Aroni.

## Zaburi 78

*Mungu Na Watu Wake*

*Utenzi wa Asafu.*

1 [e]Enyi watu wangu, sikieni mafundisho yangu,
sikilizeni maneno ya kinywa changu.
2 [f]Nitafungua kinywa changu kwa mafumbo,
nitazungumza mambo yaliyofichika, mambo ya kale:
3 [g]yale ambayo tuliyasikia na kuyajua,
yale ambayo baba zetu walituambia.
4 [h]Hatutayaficha kwa watoto wao;
tutakiambia kizazi kijacho
matendo yastahiliyo sifa ya BWANA,
uweza wake, na maajabu aliyoyafanya.
5 [i]Aliagiza amri kwa Yakobo
na akaweka sheria katika Israeli,
ambazo aliwaamuru baba zetu
wawafundishe watoto wao,
6 [j]ili kizazi kijacho kizijue,
pamoja na watoto ambao watazaliwa,
nao pia wapate kuwaeleza watoto wao.
7 [k]Ndipo wangeweka tumaini lao kwa Mungu,
nao wasingesahau matendo yake,
bali wangalizishika amri zake.
8 [l]Ili wasifanane na baba zao,
waliokuwa kizazi cha ukaidi na uasi,
ambao roho zao hazikuwa na uaminifu kwake,
ambao roho zao hazikumwamini.

9 [m]Watu wa Efraimu, ingawa walijifunga pinde,
walikimbia siku ya vita.
10 [n]Hawakulishika agano la Mungu
na walikataa kuishi kwa sheria yake.
11 [o]Walisahau aliyokuwa ameyatenda,
maajabu aliyokuwa amewaonyesha.
12 [p]Alitenda miujiza machoni mwa baba zao,
huko Soani, katika nchi ya Misri.
13 [q]Aliigawanya bahari akawapitisha,
alifanya maji yasimame imara kama ukuta.

---

[a]**77:17** Amu 5:4; Kut 9:23; Za 29:3; Kum 32:23
[b]**77:18** Za 55:8; 2Sam 22:13; Amu 5:4
[c]**77:19** Hab 3:15; Kut 14:28; 14:22; Ay 9:8; 37:23
[d]**77:20** Kut 4:16; 13:21; Za 78:52; Isa 63:11; Hes 33:1
[e]**78:1** Kut 19:5; Kum 32:29; Isa 51:4; 55:3
[f]**78:2** Za 49:4; Mt 13:35
[g]**78:3** Za 44:1; Amu 6:13
[h]**78:4** Kut 12:26; Yos 4:6, 7; Kum 4:9; 11:19; 32:7; Za 71:18; 26:7; 71:17
[i]**78:5** Za 19:7; 81:5; 147:19
[j]**78:6** Za 22:31; 102:18
[k]**78:7** Kum 6:12; 5:29
[l]**78:8** 2Nya 30:7; Kut 32:9; 23:21; Kum 21:18; Isa 30:9; 65:2
[m]**78:9** Za 78:57; 1Nya 12:2; Hos 7:16; Amu 20:39
[n]**78:10** Yos 7:10; 2Fal 17:15; Kut 16:28; Yer 11:8
[o]**78:11** Za 106:13; Isa 17:10; Yer 2:32
[p]**78:12** Neh 9:17; Za 106:22; Kut 11:9; Hes 13:22; Mwa 32:3; Isa 19:11
[q]**78:13** Kut 14:21, 22; 15:8; Za 66:6; 136:13

14 [a]Aliwaongoza kwa wingu mchana
na kwa nuru kutoka kwenye moto
usiku kucha.
15 [b]Alipasua miamba jangwani
na akawapa maji tele kama bahari,
16 [c]alitoa vijito kutoka kwenye jabali
lililochongoka,
akayafanya maji yatiririke kama
mito.

17 [d]Lakini waliendelea kutenda dhambi
dhidi yake,
wakiasi jangwani dhidi ya Aliye
Juu Sana.
18 [e]Kwa makusudi walimjaribu Mungu,
wakidai vyakula walivyovitamani.
19 [f]Walinena dhidi ya Mungu,
wakisema,
"Je, Mungu aweza kuandaa meza
jangwani?
20 [g]Alipopiga mwamba, maji yalitoka
kwa nguvu,
vijito vikatiririka maji mengi.
Lakini je, aweza kutupa chakula pia?
Je, anaweza kuwapa watu wake
nyama?"
21 [h]BWANA alipowasikia, alikasirika
sana,
moto wake ukawa dhidi ya
Yakobo,
na ghadhabu yake ikawaka dhidi
ya Israeli,
22 [i]kwa kuwa hawakumwamini Mungu,
wala kuutumainia ukombozi wake.
23 [j]Hata hivyo alitoa amri kwa anga
zilizo juu
na kufungua milango ya mbingu,
24 [k]akawanyeshea mana ili watu wale;
aliwapa nafaka ya mbinguni.
25 Watu walikula mkate wa malaika,
akawatumia chakula chote
ambacho wangeliweza kula.
26 [l]Aliachia upepo wa mashariki kutoka
kwenye mbingu
na kuuongoza upepo wa kusini
kwa uwezo wake.
27 [m]Aliwanyeshea nyama kama
mavumbi,
ndege warukao kama mchanga wa
pwani.
28 Aliwafanya washuke ndani ya kambi
yao,
kuzunguka mahema yao yote.
29 [n]Walikula na kusaza,
kwa maana alikuwa amewapa kile
walichotamani.
30 [o]Kabla hawajamaliza kula
walichokitamani,
hata kilipokuwa kingali bado
vinywani mwao,
31 [p]hasira ya Mungu ikawaka juu yao,
akawaua wale waliokuwa na
nguvu zaidi miongoni mwao,
akiwaangusha vijana wa Israeli.

32 [q]Licha ya haya yote, waliendelea
kutenda dhambi,
licha ya maajabu yake,
hawakuamini.
33 [r]Kwa hiyo akamaliza siku zao katika
ubatili
na miaka yao katika vitisho.
34 [s]Kila mara Mungu alipowaua baadhi
yao,
waliosalia walimtafuta,
walimgeukia tena kwa shauku.

---

[a]**78:14** Kut 13:21; Za 105:39
[b]**78:15** Hes 20:11; 1Kor 10:4; Kut 17; 6; Za 105:41; Isa 41:18
[c]**78:16** Kum 9:21
[d]**78:17** Za 78:32
[e]**78:18** Kut 15:24; 17:2; 1Kor 10:9; Hes 11:4
[f]**78:19** Hes 11:4; 21:5
[g]**78:20** Hes 20:11; Kut 17:6
[h]**78:21** Hes 11:1
[i]**78:22** Kum 1:32; Ebr 3:19; 3:10
[j]**78:23** Mwa 7:11; Kum 28:12; 2Fal 7:2
[k]**78:24** Kut 16:4; Yn 6:31; Neh 9:15, 20; 1Kor 10:3
[l]**78:26** Hes 11:31
[m]**78:27** Kut 16:13; Hes 11:31
[n]**78:29** Hes 11:20
[o]**78:30** Hes 11:33
[p]**78:31** Isa 10:16
[q]**78:32** Za 78:11, 17, 22
[r]**78:33** Hes 14:29, 35
[s]**78:34** Kum 4:29; Hos 5:15; Hes 5:15

35 [a]Walikumbuka kwamba Mungu
alikuwa Mwamba wao,
kwamba Mungu Aliye Juu Sana
alikuwa Mkombozi wao.
36 [b]Lakini walimdanganya kwa vinywa
vyao,
wakisema uongo kwa ndimi zao,
37 [c]mioyo yao haikuwa thabiti kwake,
wala hawakuwa waaminifu katika
agano lake.
38 [d]Hata hivyo alikuwa na huruma,
alisamehe maovu yao
na hakuwaangamiza.
Mara kwa mara alizuia hasira yake,
wala hakuchochea ghadhabu yake
yote.
39 [e]Alikumbuka kwamba wao walikuwa
nyama tu,
upepo upitao ambao haurudi.

40 [f]Mara ngapi walimwasi jangwani
na kumhuzunisha nyikani!
41 [g]Walimjaribu Mungu mara kwa
mara,
wakamkasirisha yeye Aliye
Mtakatifu wa Israeli.
42 [h]Hawakukumbuka uwezo wake,
siku aliyowakomboa kutoka kwa
mtesi,
43 [i]siku aliyoonyesha ishara zake za
ajabu huko Misri,
maajabu yake huko Soani.
44 [j]Aligeuza mito yao kuwa damu,
hawakuweza kunywa maji kutoka
vijito vyao.
45 [k]Aliwapelekea makundi ya mainzi
yakawala,
na vyura wakawaharibu.
46 [l]Aliruhusu tunutu kuharibu mimea
yao,
mazao yao kwa nzige.
47 [m]Aliharibu mizabibu yao kwa mvua
ya mawe
na mikuyu yao kwa mvua
iliyochangamana na theluji.
48 [n]Aliwaachia mifugo yao mvua ya
mawe,
akayapiga makundi ya wanyama
wao kwa radi.
49 [o]Aliwafungulia hasira yake kali,
ghadhabu yake, hasira na uadui,
na kundi la malaika wa kuharibu.
50 Aliitengenezea njia hasira yake,
hakuwaepusha na kifo,
bali aliwaachia tauni.
51 [p]Aliwapiga wazaliwa wote wa
kwanza wa Misri,
matunda ya kwanza ya ujana
katika mahema ya Hamu.
52 [q]Lakini aliwatoa watu wake kama
kundi,
akawaongoza kama kondoo
kupitia jangwani.
53 [r]Aliwaongoza salama, wala
hawakuogopa,
bali bahari iliwameza adui zao.
54 [s]Hivyo akawaleta hadi kwenye
mpaka wa nchi yake takatifu,
hadi nchi ya vilima ambayo
mkono wake wa kuume
ulikuwa umeitwaa.

[a]**78:35** Mwa 49:24; Kum 9:26
[b]**78:36** Eze 33:31
[c]**78:37** Za 78:8; Mdo 8:21
[d]**78:38** Kut 34:6; Neh 9:17; Za 25:11; 85:2; 86:15; 1Fal 21:29; Isa 1:25; 27:9; 48:9, 10; 30:18; Mik 7:18; Rum 2:4; Dan 11:35
[e]**78:39** Mwa 6:3; Isa 29:5; Ay 7:7; Yak 4:14; Yn 3:6
[f]**78:40** Kut 23:21; Za 95:8; 106:14; Efe 4:30
[g]**78:41** Kut 17:2; 2Fal 19:22; Za 71:22; 89:18
[h]**78:42** Amu 3:7; Neh 9:17; Za 27:11
[i]**78:43** Kut 10:1; 3:20
[j]**78:44** Kut 7:20, 21; Za 105:29; 78:45
[k]**78:45** Kut 8:2, 6, 24; Za 105
[l]**78:46** Nah 3:15; Kut 10:13
[m]**78:47** Za 105:32; 147:17; Kut 9:23
[n]**78:48** Kut 9:25
[o]**78:49** Kut 15:7; Mwa 19:13; 1Kor 10:10; Rum 2:8
[p]**78:51** Mwa 9:12; Kut 12:12; Za 135:8; 105:23; 106:22
[q]**78:52** Ay 21:11; Za 28:9; 77:20
[r]**78:53** Kut 14:28; 15:7; Za 106:10
[s]**78:54** Kut 15:17; Za 44:3

55 [a]Aliyafukuza mataifa mbele yao,
na kuwagawia nchi zao kama urithi,
aliwakalisha makabila ya Israeli katika makao yao.

56 Lakini wao walimjaribu Mungu,
na kuasi dhidi ya Yeye Aliye Juu Sana,
wala hawakuzishika sheria zake.
57 [b]Kama baba zao, hawakuwa thabiti wala waaminifu,
wakawa wasioweza kutegemewa
kama upinde wenye kasoro.
58 [c]Wakamkasirisha Mungu kwa mahali pao pa juu pa kuabudia miungu,
wakachochea wivu wake kwa sanamu zao.
59 [d]Wakati Mungu alipowasikia, alikasirika sana,
akamkataa Israeli kabisa.
60 [e]Akaiacha hema ya Shilo,
hema aliyokuwa ameiweka katikati ya wanadamu.
61 [f]Akalipeleka Sanduku la nguvu zake utumwani,
utukufu wake mikononi mwa adui.
62 [g]Aliachia watu wake wauawe kwa upanga,
akaukasirikia sana urithi wake.
63 [h]Moto uliwaangamiza vijana wao,
na wanawali wao hawakuimbiwa nyimbo za arusi,
64 [i]makuhani wao waliuawa kwa upanga,
wala wajane wao hawakuweza kulia.

65 [j]Ndipo Bwana alipoamka kama vile kuamka usingizini,
kama vile mtu aamkavyo kutoka kwenye bumbuazi la mvinyo.
66 [k]Aliwapiga na kuwashinda adui zake,
akawatia katika aibu ya milele.
67 [l]Ndipo alipozikataa hema za Yosefu,
hakulichagua kabila la Efraimu,
68 [m]lakini alilichagua kabila la Yuda,
Mlima Sayuni, ambao aliupenda.
69 [n]Alijenga patakatifu pake kama vilele,
kama dunia ambayo aliimarisha milele.
70 [o]Akamchagua Daudi mtumishi wake
na kumtoa kwenye mazizi ya kondoo.
71 [p]Kutoka kuchunga kondoo alimleta
kuwa mchungaji wa watu wake Yakobo,
wa Israeli urithi wake.
72 [q]Naye Daudi aliwachunga kwa uadilifu wa moyo,
kwa mikono ya ustadi aliwaongoza.

## Zaburi 79

*Maombi Kwa Ajili Ya Wokovu Wa Taifa*

*Zaburi ya Asafu.*

1 [r]Ee Mungu, mataifa yameuvamia urithi wako,
wamelinajisi Hekalu lako takatifu,
wameifanya Yerusalemu kuwa magofu.

---

[a]**78:55** Za 44:2; Kum 1:38; Yos 13:7; Mdo 13:19
[b]**78:57** 2Nya 30:7; Za 78:9; Eze 20:27; Hos 7:16
[c]**78:58** Amu 2:12; Law 26:30; Kut 20:4; Kum 12:2; 5:8; 32:21; Hes 33:51
[d]**78:59** Za 55:19; Law 26:28; Hes 32:14; Kum 32:19; Ebr 4:13
[e]**78:60** Yos 18:1; Eze 8:6; 1Sam 4:11; Yer 7:12
[f]**78:61** Amu 18:30; 1Sam 4:12; Za 132:8; 1Sam 4:17
[g]**78:62** Kum 28:25; 1Sam 10:1
[h]**78:63** 1Fal 4:32; Yer 7:32; 16:9; 25:10; Hes 11:1
[i]**78:64** Ay 27:15; 1Sam 4:17
[j]**78:65** Za 44:23; Isa 42:13
[k]**78:66** 1Sam 5:6
[l]**78:67** Yer 7:15; Hos 9:13; 12:1
[m]**78:68** Hes 1:7; Kut 15:17; Za 68:16; 108:8
[n]**78:69** Za 15:1; 1Fal 6:1
[o]**78:70** 1Sam 16:1
[p]**78:71** Mwa 37:2; Za 28:9; 2Sam 5:2; 1Nya 11:2; Mik 5:2-4; Zek 11:4
[q]**78:72** 1Fal 9:4; Mwa 17:1
[r]**79:1** Kut 34:9; Law 20:3; 2Fal 25:9; Neh 4:2; Isa 6:11; Yer 26:18

2 [a]Wametoa maiti za watumishi
kuwa chakula cha ndege wa
angani
na nyama ya watakatifu wako
kwa wanyama wa nchi.
3 [b]Wamemwaga damu kama maji
kuzunguka Yerusalemu yote,
wala hakuna yeyote wa kuwazika.
4 [c]Tumekuwa kitu cha aibu kwa jirani
zetu,
cha dharau na mzaha kwa wale
wanaotuzunguka.

5 [d]Hata lini, Ee BWANA? Je, wewe
utakasirika milele?
Wivu wako utawaka kama moto
hadi lini?
6 [e]Mwaga ghadhabu yako kwa mataifa
yasiyokukubali,
juu ya falme za hao wasioliitia
jina lako,
7 [f]kwa maana wamemrarua Yakobo
na kuharibu nchi ya makao yake.
8 [g]Usituhesabie dhambi za baba zetu,
huruma yako na itujie hima,
kwa maana tu wahitaji mno.

9 [h]Ee Mungu Mwokozi wetu, utusaidie,
kwa ajili ya utukufu wa jina lako;
tuokoe na kutusamehe dhambi zetu
kwa ajili ya jina lako.
10 [i]Kwa nini mataifa waseme,
"Yuko wapi Mungu wenu?"
Mbele ya macho yetu,
dhihirisha kati ya mataifa
kwamba unalipiza kisasi damu
iliyomwagwa
ya watumishi wako.
11 [j]Kilio cha huzuni cha wafungwa
kifike mbele zako;
kwa nguvu za mkono wako
hifadhi wale waliohukumiwa kufa.

12 [k]Walipize jirani zetu mara saba
vifuani mwao
aibu walizovurumisha juu yako,
Ee BWANA.
13 [l]Ndipo sisi watu wako, kondoo wa
malisho yako,
tutakusifu milele;
toka kizazi hadi kizazi
tutasimulia sifa zako.

## Zaburi 80

*Maombi Kwa Ajili Ya Kuponywa Kwa Taifa*

*Kwa mwimbishaji. Mtindo wa "Yungiyungi za Agano." Zaburi ya Asafu.*

1 [m]Ee Mchungaji wa Israeli tusikie,
wewe umwongozaye Yosefu kama
kundi;
wewe uketiye katika kiti cha enzi
katikati ya makerubi, angaza
2 [n]mbele ya Efraimu, Benyamini na
Manase.
Uamshe nguvu zako,
uje utuokoe.

3 [o]Ee Mungu, uturejeshe,
utuangazie uso wako,
ili tuweze kuokolewa.

4 [p]Ee BWANA Mungu Mwenye Nguvu
Zote,
hata lini hasira yako itawaka na
kufoka moshi
dhidi ya maombi ya watu wako?

---

[a]**79:2** Ufu 19:17-18; Kum 28:26; Yer 7:33
[b]**79:3** Ufu 11:9; Yer 25:33; 16:4
[c]**79:4** Eze 5:14; Za 39:8; 44:13
[d]**79:5** Za 74:10; 74:1; 85:5; Kum 29:20; Za 89:46; Sef 3:8; Eze 36:5
[e]**79:6** Ufu 16:1; Za 2:5; 110:5; 14:4; 53:4; 147:20; 69:24; Yer 10:25; Isa 45:4
[f]**79:7** Isa 9:12; Yer 10:25
[g]**79:8** Mwa 9:25; Yer 44:21; Za 116:6; 142:6
[h]**79:9** 2Nya 14:11; 25:11; 31:3; Yer 14:7; Yos 7:9
[i]**79:10** Za 42:3; 94:1; Ufu 6:10; Za 79:3
[j]**79:11** Hes 14:17
[k]**79:12** Isa 65:6; Yer 32:18; Mwa 4:15
[l]**79:13** Za 44:8; 74:1; Isa 43:21
[m]**80:1** Kut 25:22; 1Sam 4:4; Za 77:20; 89:1; Kum 33:2
[n]**80:2** Hes 2:18-24; Za 35:23; 54:1; 71:2; 109:26; 116:4; 119:94
[o]**80:3** Za 71:20; 85:4; Yer 31:18; Mao 5:21; Hes 6:25; Za 80:7, 19; 1Fal 18:37
[p]**80:4** Za 74:10; Kum 29:20

5 [a]Umewalisha kwa mkate wa
machozi,
umewafanya wanywe machozi
bakuli tele.
6 [b]Tumekuwa chanzo cha ugomvi kwa
jirani zetu,
na adui zetu wanatudhihaki.

7 [c]Ee Mungu Mwenye Nguvu Zote,
uturejeshe;
utuangazie uso wako,
nasi tuweze kuokolewa.

8 [d]Ulileta mzabibu kutoka Misri,
ukawafukuza mataifa, ukaupanda.
9 Uliandaa shamba kwa ajili yake,
mizizi ikawa imara, ukajaza nchi.
10 Milima ilifunikwa kwa kivuli chake,
matawi yake yakafunika mierezi
mikubwa.
11 [e]Matawi yake yalienea mpaka
Baharini,[f]
machipukizi yake mpaka kwenye
Mto.[g]

12 [h]Mbona umebomoa kuta zake
ili wote wapitao karibu
wazichume zabibu zake?
13 [i]Nguruwe mwitu wanauharibu
na wanyama wa kondeni hujilisha
humo.
14 [j]Turudie, Ee Mungu Mwenye Nguvu
Zote!
Tazama chini kutoka mbinguni na
uone!
Linda mzabibu huu,
15 [k]mche ulioupanda kwa mkono
wako wa kuume,
mwana uliyemlea
kwa ajili yako mwenyewe.

16 [l]Mzabibu wako umekatwa,
umechomwa moto,
unapowakemea, watu wako
huangamia.
17 [m]Mkono wako na utulie juu ya mtu
aliyeko mkono wako wa
kuume,
mwana wa mtu uliyemlea kwa
ajili yako mwenyewe.
18 [n]Ndipo hatutakuacha tena,
utuhuishe, nasi tutaliitia jina lako.

19 [o]Ee BWANA Mungu Mwenye Nguvu
Zote, uturejeshe;
utuangazie uso wako,
ili tuweze kuokolewa.

## Zaburi 81

*Wimbo Wa Sikukuu*

*Kwa mwimbishaji. Mtindo wa gitithi.*
*Zaburi ya Asafu.*

1 [p]Mwimbieni kwa furaha, Mungu
aliye nguvu yetu;
mpigieni kelele za shangwe
Mungu wa Yakobo!
2 [q]Anzeni wimbo, pigeni matari,
pigeni kinubi na zeze kwa sauti
nzuri.

3 [r]Pigeni baragumu za pembe za
kondoo dume
wakati wa Mwandamo wa Mwezi,
na wakati wa mwezi mpevu,
katika siku ya Sikukuu yetu;
4 [s]hii ni amri kwa Israeli,
agizo la Mungu wa Yakobo.

---

[a]**80:5** Ay 3:24; Isa 30:20
[b]**80:6** Za 79:4
[c]**80:7** Za 80:3
[d]**80:8** Isa 5:1-2, 7; Yer 2:21; Mt 21:33-41; Kut 15:17; 23:28-30; Yos 13:6; Mdo 7:45; Eze 15:6
[e]**80:11** Kut 23:31; Za 72:8
[f]11 Huenda inamaanisha Bahari ya Mediterania.
[g]11 Yaani Mto Frati.
[h]**80:12** Isa 5:5; 30:13; Za 89:40; Yer 39:8
[i]**80:13** Yer 5:6
[j]**80:14** Kum 26:15; Zek 1:12, 16, 17; Isa 63:15
[k]**80:15** Isa 49:5
[l]**80:16** Za 79:1; Kum 28:20
[m]**80:17** Ay 25:6; Za 89:21; 110:1; Kut 4:22; Dan 7:13, 14; Yn 5:21-27
[n]**80:18** Za 85:6; Isa 57:15; Hos 6:2
[o]**80:19** Hes 6:25; Za 27:4, 9
[p]**81:1** Za 66:1; 81:4
[q]**81:2** Kut 15:20; Za 92:3; Ay 21:12
[r]**81:3** Kut 19:13; Neh 10:33
[s]**81:4** Za 81:1; Law 23:24; Hes 10:10

5 [a]Aliiweka iwe kama sheria kwa
Yosefu
alipotoka dhidi ya Misri,
huko tulikosikia lugha ambayo
hatukuielewa.

6 [b]Asema, "Nimeondoa mzigo
mabegani mwao;
mikono yao iliwekwa huru kutoka
kwenye kikapu.
7 [c]Katika shida yako uliniita nami
nikakuokoa,
nilikujibu katika mawingu yenye
ngurumo;
nilikujaribu katika maji ya Meriba.

8 [d]"Enyi watu wangu, sikieni, nami
nitawaonya:
laiti kama mngenisikiliza, ee
Israeli!
9 [e]Hamtakuwa na mungu mgeni
miongoni mwenu;
msimsujudie mungu wa kigeni.
10 [f]Mimi ni BWANA Mungu wako,
niliyekutoa nchi ya Misri.
Panua sana kinywa chako
nami nitakijaza.

11 [g]"Lakini watu wangu hawakutaka
kunisikiliza;
Israeli hakutaka kunitii.
12 [h]Basi niliwaacha katika ukaidi wa
mioyo yao
wafuate mashauri yao wenyewe.

13 [i]"Laiti kama watu wangu
wangalinisikiliza,
kama Israeli wangalifuata njia
zangu,
14 [j]ningaliwatiisha adui zao kwa
haraka,
na kuugeuza mkono wangu dhidi
ya watesi wao!
15 [k]Wale wanaomchukia BWANA
wangalinyenyekea mbele
zake,
na adhabu yao ingedumu milele.
16 [l]Bali ninyi mngalilishwa ngano iliyo
bora,
na kuwatosheleza kwa asali
itokayo kwenye mwamba."

## Zaburi 82

*Maombi Kwa Ajili Ya Kutaka Haki*

*Zaburi ya Asafu.*

1 [m]Mungu anaongoza kusanyiko kuu,
anatoa hukumu miongoni mwa
"miungu":

2 [n]"Hata lini utaendelea kuwatetea
wasio haki
na kuonyesha upendeleo kwa
waovu?
3 [o]Teteeni wanyonge na yatima,
tunzeni haki za maskini na
walioonewa.
4 Mwokoeni mnyonge na mhitaji,
wakomboeni kutoka mkononi
mwa mwovu.

5 [p]"Hawajui lolote, hawaelewi lolote.
Wanatembea gizani;
misingi yote ya dunia imetikisika.

6 [q]"Nilisema, 'Ninyi ni "miungu";
ninyi nyote ni wana wa Aliye Juu
Sana.'

---

[a]**81:5** Kut 11:4; Za 114:1
[b]**81:6** Kut 1:14; Isa 9:4; 52:2
[c]**81:7** Kut 2:23; 19:19; 17:7; Kum 33:8
[d]**81:8** Za 50:7; 78:1
[e]**81:9** Kut 20:3
[f]**81:10** Kut 6:6; 13:3; 29:46; Eze 2:8; Za 107:9; 37:3; Yn 13:7
[g]**81:11** Kut 32:1-6
[h]**81:12** Eze 20:25; Mdo 7:42; Rum 1:24
[i]**81:13** Kum 5:29; Isa 48:18; Yer 44:4, 5; Mt 23:37
[j]**81:14** Za 47:3; Amo 1:8
[k]**81:15** 2Sam 22:45
[l]**81:16** Kum 32:14
[m]**82:1** Mhu 5:8; Kut 21:6; Za 7:8; 58:11; Isa 3; 13; 66:16; Yoe 3:12; Ay 21:22
[n]**82:2** Kum 1:17; Za 58:1-2; Mit 18:5
[o]**82:3** Kum 24:17; Za 140:12; Yer 5:28; 22:16
[p]**82:5** Za 11:3; 14:4; 53:2; Ay 30:26; Isa 5:30; 8:21-22; 9:2; 59:9; 60:2; Yer 13:16; 23:12, 16; Mao 3:2; Amu 5:4
[q]**82:6** Kut 22:9; Yn 10:34

7 [a]Lakini mtakufa kama wanadamu wa kawaida;
mtaanguka kama mtawala mwingine yeyote."

8 [b]Ee Mungu, inuka uihukumu nchi,
kwa kuwa mataifa yote ni urithi wako.

## Zaburi 83

*Maombi Kwa Ajili Ya Kushindwa Kwa Adui Wa Israeli*

*Wimbo. Zaburi ya Asafu.*

1 [c]Ee Mungu, usinyamaze kimya,
usinyamaze, Ee Mungu, usitulie.
2 [d]Tazama watesi wako wanafanya fujo,
jinsi adui zako wanavyoinua vichwa vyao.
3 [e]Kwa hila, wanafanya shauri dhidi ya watu wako,
wanafanya shauri baya dhidi ya wale unaowapenda.
4 [f]Wanasema, "Njooni, tuwaangamize kama taifa,
ili jina la Israeli lisikumbukwe tena."

5 [g]Kwa nia moja wanapanga mashauri mabaya pamoja,
wanafanya muungano dhidi yako,
6 [h]mahema ya Edomu na Waishmaeli,
ya Wamoabu na Wahagari,
7 [i]Gebali,[j] Amoni na Amaleki,
Ufilisti, pamoja na watu wa Tiro.
8 [k]Hata Ashuru wameungana nao
kuwapa nguvu wazao wa Loti.

9 [l]Uwatendee kama vile ulivyowatendea Midiani,
na kama vile ulivyowatendea Sisera na Yabini
hapo kijito cha Kishoni,
10 [m]ambao waliangamia huko Endori
na wakawa kama takataka juu ya nchi.
11 [n]Wafanye wakuu wao kama Orebu na Zeebu,
watawala wao kama Zeba na Salmuna,
12 [o]ambao walisema, "Na tumiliki nchi
ya malisho ya Mungu."

13 [p]Ee Mungu wangu, wapeperushe kama mavumbi ya kisulisuli,
kama makapi yapeperushwayo na upepo.
14 [q]Kama vile moto uteketezavyo msitu
au mwali wa moto unavyounguza milima,
15 [r]wafuatilie kwa tufani yako
na kuwafadhaisha kwa dhoruba yako.
16 [s]Funika nyuso zao kwa aibu
ili watu walitafute jina lako, Ee Bwana.

17 [t]Wao na waaibishwe na kufadhaishwa milele,
na waangamie kwa aibu.
18 [u]Hebu wajue kwamba wewe, ambaye jina lako ni Bwana,
kwamba wewe peke yako ndiwe Uliye Juu Sana ya dunia yote.

---

[a]**82:7** Za 49:12; Eze 31:14
[b]**82:8** Za 12:5; 76:9; 2:8
[c]**83:1** Za 28:1; 35:22; Isa 42:14; 57:11; 62:1; 64:12
[d]**83:2** Za 2:1; Isa 17:12; Amu 8:28
[e]**83:3** Kut 1:10; Za 31:13; 17:14
[f]**83:4** Es 3:6; Yer 33:24; 11:19; 2Sam 10:6; 2Nya 20:1
[g]**83:5** Za 2:2
[h]**83:6** Za 137:7; Isa 34:5; Yer 49:7; Amo 1:11; 2Nya 20:1; Mwa 25:16
[i]**83:7** Yos 13:5; Mwa 19:38; 14:7; Kut 17:14; 15:14; Isa 23:3; Eze 27:3
[j]7 Yaani Bubilo, mji wa zamani sana wa Ufoinike (kama kilomita 80 kaskazini mwa Beiruti).
[k]**83:8** Mwa 10:11; Kum 2:9
[l]**83:9** Hes 31:7, 8; Isa 9:4; Yos 11:1; Amu 4:2, 15, 23, 24; 7:1, 2, 3; Mwa 25:2
[m]**83:10** 1Sam 28:7; 2Fal 9:37; Isa 5:25; Yer 8:2; 9:22; 16:4; 25:33; Sef 1:17
[n]**83:11** Amu 7:25; 8:5
[o]**83:12** 2Nya 20:11; Eze 35:10
[p]**83:13** Ay 13:25
[q]**83:14** Kum 32:22; Isa 9:13
[r]**83:15** Za 50:3; Ay 9:17
[s]**83:16** Za 34:5; 109:29; 132:18
[t]**83:17** 2Fal 19:26; Za 35:4
[u]**83:18** Za 68:4; 7:8; 18:13

## Zaburi 84

*Kuionea Shauku Nyumba Ya Mungu*

*Kwa mwimbishaji. Mtindo wa gitithi. Zaburi ya wana wa Kora.*

1 [a]Ee BWANA Mwenye Nguvu Zote,
makao yako yapendeza kama nini!
2 [b]Nafsi yangu inatamani sana,
naam, hata kuona shauku,
kwa ajili ya nyua za BWANA;
moyo wangu na mwili wangu
vinamlilia Mungu Aliye Hai.

3 [c]Hata shomoro amejipatia makao,
mbayuwayu amejipatia kiota
mahali awezapo kuweka makinda yake:
mahali karibu na madhabahu yako,
Ee BWANA Mwenye Nguvu Zote,
Mfalme wangu na Mungu wangu.
4 Heri wale wanaokaa nyumbani mwako,
wanaokusifu wewe daima.

5 [d]Heri wale ambao nguvu zao ziko kwako,
na njia ziendazo Sayuni zimo mioyoni mwao.
6 [e]Wanapopita katika Bonde la Baka,[f]
hulifanya mahali pa chemchemi,
pia mvua za vuli hulijaza kwa madimbwi.[g]
7 [h]Huendelea toka nguvu hadi nguvu,
hadi kila mmoja afikapo
mbele za Mungu huko Sayuni.

8 [i]Ee BWANA Mungu Mwenye Nguvu Zote, sikia maombi yangu;
nisikilize, Ee Mungu wa Yakobo.
9 [j]Ee Mungu, uitazame ngao yetu,
mtazame kwa wema mpakwa mafuta wako.
10 [k]Siku moja katika nyua zako ni bora
kuliko siku elfu mahali pengine;
afadhali ningekuwa bawabu katika nyumba ya Mungu wangu
kuliko kukaa katika mahema ya waovu.
11 [l]Kwa kuwa BWANA ni jua na ngao,
BWANA hutoa wema na heshima;
hakuna kitu chema anachowanyima
wale ambao hawana hatia.

12 [m]Ee BWANA Mwenye Nguvu Zote,
heri ni mtu yule anayekutumaini wewe.

## Zaburi 85

*Maombi Kwa Ajili Ya Ustawi Wa Taifa*

*Kwa mwimbishaji. Zaburi ya wana wa Kora.*

1 [n]Ee BWANA, ulionyesha wema kwa nchi yako.
Ulimrejeshea Yakobo baraka zake.[o]
2 [p]Ulisamehe uovu wa watu wako,
na kufunika dhambi zao zote.
3 [q]Uliweka kando ghadhabu yako yote
na umegeuka na kuiacha hasira yako kali.

4 [r]Ee Mungu Mwokozi wetu,
uturejeshe tena,
nawe uiondoe chuki yako juu yetu.
5 [s]Je, utatukasirikia milele?
Utaendeleza hasira yako kwa vizazi vyote?
6 [t]Je, hutatuhuisha tena,
ili watu wako wakufurahie?

---

[a]**84:1** Kum 33:27; Za 27:4; 43:3; 90:1; 132:5; 26:8; 27:4; Ebr 9:23; Ufu 21:2, 3
[b]**84:2** Ay 19:27; Yos 3:10
[c]**84:3** Za 2:6; 5:2; 43:4; Yer 44:11
[d]**84:5** Za 81:1; Yer 31:6
[e]**84:6** Ay 38:26; Yoe 2:23
[f]6 Yaani Bonde la Vilio.
[g]6 Au: baraka.
[h]**84:7** Ay 17:9; Kum 16:16; 1Fal 8:1
[i]**84:8** Za 4:1
[j]**84:9** 1Sam 16:6; Za 2:2; 59:11; 18:50; 132:17
[k]**84:10** 1Nya 23:5
[l]**84:11** Isa 60:19; Yer 43:13; Ufu 21:23; Mwa 15:1; Za 34:10
[m]**84:12** Za 2:12
[n]**85:1** Kum 30:3; Za 14:7; Yer 30:18; Eze 39:25
[o]1 Au: Uliwarudisha mateka wa Yakobo.
[p]**85:2** Hes 14:19; Kut 32:30; Za 78:38
[q]**85:3** Za 78:38; 106:23; Dan 9:16; Kut 32:12; Yn 3:9; Kum 13:17
[r]**85:4** Za 71:20; 65:5
[s]**85:5** Za 50:21
[t]**85:6** Za 80:18; Flp 3:1; Hab 3:2

7 [a]Utuonyeshe upendo wako usiokoma,
Ee BWANA,
utupe wokovu wako.

8 [b]Nitasikiliza lile atakalosema Mungu
aliye BWANA;
anaahidi amani kwa watu wake,
watakatifu wake:
lakini nao wasirudie upumbavu.
9 [c]Hakika wokovu wake uko karibu na
wale wamchao,
ili utukufu wake udumu katika
nchi yetu.

10 [d]Upendo na uaminifu hukutana
pamoja,
haki na amani hubusiana.
11 [e]Uaminifu huchipua kutoka nchi,
haki hutazama chini kutoka
mbinguni.
12 [f]Naam, hakika BWANA atatoa kilicho
chema,
nayo nchi yetu itazaa mavuno
yake.
13 Haki itatangulia mbele yake
na kutengeneza njia kwa ajili ya
hatua zake.

## Zaburi 86

*Kuomba Msaada*

*Maombi ya Daudi.*

1 [g]Ee BWANA, sikia na unijibu,
kwa maana mimi ni maskini na
mhitaji.
2 [h]Linda maisha yangu, kwa maana
nimejiweka kwako,
wewe ni Mungu wangu,
mwokoe mtumishi wako
anayekutumaini.
3 [i]Ee BWANA, nihurumie mimi,
kwa maana ninakuita mchana
kutwa.
4 [j]Mpe mtumishi wako furaha,
kwa kuwa kwako wewe, Ee
BWANA,
ninainua nafsi yangu.

5 [k]Ee BWANA, wewe ni mwema na
mwenye kusamehe,
umejaa upendo kwa wote
wakuitao.
6 [l]Ee BWANA, sikia maombi yangu,
sikiliza kilio changu unihurumie.
7 [m]Katika siku ya shida yangu
nitakuita,
kwa maana wewe utanijibu.

8 [n]Ee BWANA, katikati ya miungu
hakuna kama wewe,
hakuna matendo ya kulinganishwa
na yako.
9 [o]Ee BWANA, mataifa yote
uliyoyafanya
yatakuja na kuabudu mbele zako;
watalileteea utukufu jina lako.
10 [p]Kwa maana wewe ni mkuu, na
unafanya mambo ya ajabu;
wewe peke yako ndiwe Mungu.

---

[a]**85:7** Za 6:4; 27:1
[b]**85:8** Law 26:6; Isa 60:17; Yn 14:27; 2The 3:16; Mit 26:11; 27:22; Hab 2:1; Zek 9:10; 2Pet 2:20
[c]**85:9** Za 27:1; Kut 29:43; Isa 43:3; 45:8; 46:13; 62:11; 51:5; 56:1; 60:19; Hag 2:9; Zek 2:5
[d]**85:10** Isa 32:17; Mit 3:3; Lk 2:14; Yn 1:17; 14:27; Za 89:14; 115:1; 72:2, 3; Mik 7:20
[e]**85:11** Isa 45:8
[f]**85:12** Za 67:6; 84:11; Yak 1:17; Law 26:4; Zek 8:12
[g]**86:1** Za 17:6
[h]**86:2** Za 25:2; 31:14
[i]**86:3** Za 4:1; 9:13; 57:1; 88:9
[j]**86:4** Za 46:5; 143:8
[k]**86:5** Yoe 2:13; Yon 4:2; Neh 9:17; Za 103:8; 145:8; 130:7, 8; Kut 34:6
[l]**86:6** Za 5:2; 17:1
[m]**86:7** Za 3:4; 4:3; 27:5; 50:15; 94:13; 80:18; 91:15; Isa 30:19; 58:9; 65:24; Ay 22:27; Zek 13:9; Hab 3:16
[n]**86:8** Ay 21:22; Za 18:31; 1Sam 2:2; Kut 8:10; 15:11; Kum 3:24; 2Sam 7:22
[o]**86:9** Za 65:2; 66:4; Isa 19:21; 27:13; 49:7; Zek 8:20-22; 14:6; Ufu 15:4; Isa 43:7; 44:23; Za 95:6, 7
[p]**86:10** 2Sam 7:22; Kut 3:20; Kum 6:4; Za 48:1; 71:17; 72:18; 1Kor 8:4; Isa 37:16; 43:10; Mk 12:29; Efe 4:6

11 [a]Ee BWANA, nifundishe njia yako,
nami nitakwenda katika kweli yako;
nipe moyo usiositasita,
ili niweze kulicha jina lako.
12 [b]Ee BWANA wangu, nitakusifu kwa moyo wote;
nitaliadhimisha jina lako milele.
13 [c]Kwa maana upendo wako ni mkuu kwangu;
umeniokoa kutoka kwenye vilindi vya kaburi.[d]

14 [e]Ee Mungu, wenye majivuno wananishambulia;
kundi la watu wakatili linatafuta uhai wangu:
watu wasiokuheshimu wewe.
15 [f]Lakini wewe, Ee BWANA, ni Mungu wa huruma na neema,
si mwepesi wa hasira, bali ni mwingi wa upendo na uaminifu.
16 [g]Nigeukie na unihurumie;
mpe mtumishi wako nguvu zako,
mwokoe mwana wa mtumishi wako wa kike.[h]
17 [i]Nipe ishara ya wema wako,
ili adui zangu waione nao waaibishwe,
kwa kuwa wewe, Ee BWANA,
umenisaidia na kunifariji.

## Zaburi 87

*Sifa Za Yerusalemu*

*Zaburi ya wana wa Kora. Wimbo.*

1 [j]Ameuweka msingi wake katika mlima mtakatifu;
2 [k]BWANA anayapenda malango ya Sayuni
kuliko makao yote ya Yakobo.
3 [l]Mambo matukufu yanasemwa juu yako,
ee mji wa Mungu:
4 [m]"Nitaweka kumbukumbu ya Rahabu[n] na Babeli
miongoni mwa wale wanaonikubali mimi:
Ufilisti pia na Tiro, pamoja na Kushi,[o]
nami nitasema, 'Huyu alizaliwa Sayuni.' "

5 [p]Kuhusu Sayuni itasemwa hivi,
"Huyu na yule walizaliwa humo,
naye Aliye Juu Sana mwenyewe atamwimarisha."
6 [q]BWANA ataandika katika orodha ya mataifa:
"Huyu alizaliwa Sayuni."
7 [r]Watakapokuwa wanapiga vinanda wataimba,
"Chemchemi zangu zote ziko kwako."

---

[a]**86:11** Kut 33:13; 1Sam 12:23; Za 25:5; Eze 11:19; Za 26:3; Kum 6:24; Yer 24:7; 32:39; 1Kor 7:35
[b]**86:12** Za 9:1
[c]**86:13** Za 56:13; 116:8; 34:4; 49:15; 16:10
[d]13 Yaani Kuzimu.
[e]**86:14** Za 54:3
[f]**86:15** Za 116:5; 103:8; 111:4; 145:8; 51:1; Hes 14:18; Za 86:5; Kut 34:6; Yoe 2:13; Neh 9:17
[g]**86:16** Za 6:4; 9:13; 18:1; 116:16
[h]16 Au: mwokoe mwanao mwaminifu.
[i]**86:17** Kut 3:12; Mt 24:3; Yn 2:11

[j]**87:1** Za 48:1
[k]**87:2** Za 2:6
[l]**87:3** Za 46:4; Isa 60:1
[m]**87:4** Ay 9:13; 2Sam 8:1; Za 83:7; 45:12; Yoe 3:4; Isa 19:25
[n]4 Rahabu hapa ni jina la ushairi la Misri.
[o]4 Kushi hapa ina maana ya Naili ya juu, yaani Ethiopia.
[p]**87:5** Eze 48:35; Mt 16:18
[q]**87:6** Isa 4:3; Kut 32:32; Yer 3:19; Eze 13:9; Za 22:30; 69:28; Mal 3:16
[r]**87:7** Za 149:3; 36:9

## Zaburi 88

*Kilio Kwa Ajili Ya Kuomba Msaada*

*Wimbo. Zaburi ya wana wa Kora. Kwa mwimbishaji. Mtindo wa mahalathi leanothi. Utenzi wa Hemani Mwezrahi.*

1 [a]Ee BWANA, Mungu uniokoaye,
nimelia mbele zako usiku na mchana.
2 Maombi yangu yafike mbele zako,
utegee kilio changu sikio lako.

3 [b]Kwa maana nafsi yangu imejaa taabu,
na maisha yangu yanakaribia kaburi.[c]
4 [d]Nimehesabiwa miongoni mwa wale waendao shimoni,
niko kama mtu asiye na nguvu.
5 [e]Nimetengwa pamoja na wafu,
kama waliochinjwa walalao kaburini,
ambao huwakumbuki tena,
ambao wamekatiliwa mbali na uangalizi wako.

6 [f]Umenitupa katika shimo lenye kina kirefu sana,
katika vina vya giza nene.
7 [g]Ghadhabu yako imekuwa nzito juu yangu,
umenigharikisha kwa mawimbi yako yote.

8 [h]Umenitenga na rafiki zangu wa karibu
na kunifanya chukizo kwao.
Nimezuiliwa, wala siwezi kutoroka;
9 [i]nuru ya macho yangu
imefifia kwa ajili ya huzuni.
Ee BWANA, ninakuita kila siku,
ninakunyooshea wewe mikono yangu.
10 [j]Je, wewe huwaonyesha wafu maajabu yako?
Je, wale waliokufa huinuka na kukusifu?

11 [k]Je, upendo wako hutangazwa kaburini,
uaminifu wako katika Uharibifu?[l]
12 [m]Je, maajabu yako hujulikana mahali pa giza,
au matendo yako ya haki katika nchi ya usahaulifu?

13 [n]Lakini ninakulilia wewe, Ee BWANA, unisaidie;
asubuhi maombi yangu huja mbele zako.
14 [o]Ee BWANA, kwa nini unanikataa
na kunificha uso wako?

15 [p]Tangu ujana wangu nimeteseka, nikakaribia kifo;
nimepatwa na hofu zako, nami nimekata tamaa.
16 [q]Ghadhabu yako imepita juu yangu;
hofu zako zimeniangamiza.
17 [r]Mchana kutwa zinanizunguka kama mafuriko;
zimenimeza kabisa.
18 [s]Umeniondolea marafiki na wapendwa wangu;
giza limekuwa ndilo rafiki yangu wa karibu kuliko wote.

---

[a]**88:1** Za 51:14; 3:4; 22:2; Lk 18:7
[b]**88:3** Ay 33:22; Isa 38:10; Za 6:3; 25:17; 107:18
[c]3 Kaburi hapa maana yake ni Kuzimu, kwa Kiebrania ni Sheol.
[d]**88:4** Za 31:12; 18:1
[e]**88:5** Za 31:22
[f]**88:6** Za 30:1; 69:15; Mao 3:55; Yon 2:3
[g]**88:7** Za 7:11; 42:7
[h]**88:8** Ay 3:23; 19:13; Za 31:11; Yer 32:2; 33:1
[i]**88:9** Za 38:10; 5:2; 143:6; Ay 11:13
[j]**88:10** Za 6:5
[k]**88:11** Za 30:9
[l]11 Yaani *Abadon.*
[m]**88:12** Ay 10:21; 31:12; Mhu 8:10
[n]**88:13** Za 30:2; 5:3; 55:17; 119:147
[o]**88:14** Za 43:2; 13:1
[p]**88:15** Dan 9:26; Za 9:12; 129:1; Yer 22:21; Eze 16:22; Hos 2:15; Isa 53:8; Ay 6:4; 18:11; 2Kor 4:8
[q]**88:16** Za 7:11; Ay 6:4
[r]**88:17** Za 124:4
[s]**88:18** Za 88:8; 38:11; Ay 19:13

## Zaburi 89

*Wimbo Wakati Wa Taabu Ya Kitaifa*

*Utenzi wa Ethani Mwezrahi.*

1 [a]Nitaimba juu ya upendo mkuu wa
BWANA milele;
kwa kinywa changu nitajulisha
uaminifu wako
ujulikane kwa vizazi vyote.
2 [b]Nitatangaza kuwa upendo wako
unasimama imara milele
na uaminifu wako umeuthibitisha
mbinguni.

3 [c]Ulisema, "Nimefanya agano na
mteule wangu,
nimemwapia mtumishi wangu
Daudi,
4 [d]'Nitaimarisha uzao wako milele
na kudumisha ufalme wako kwa
vizazi vyote.' "

5 [e]Ee BWANA, mbingu zinayasifu
maajabu yako,
uaminifu wako pia katika
kusanyiko la watakatifu.
6 [f]Kwa kuwa ni nani katika mbingu
anayeweza kulinganishwa na
BWANA?
Ni nani miongoni mwa viumbe vya
mbinguni
aliye kama BWANA?
7 [g]Katika kusanyiko la watakatifu,
Mungu huogopwa sana,
anahofiwa kuliko wote
wanaomzunguka.
8 [h]Ee BWANA Mwenye Nguvu Zote,
ni nani aliye kama wewe?
Ee BWANA, wewe ni mwenye nguvu,
na uaminifu wako unakuzunguka.
9 [i]Wewe unatawala bahari yenye
msukosuko;
wakati mawimbi yake
yanapoinuka, wewe
unayatuliza.
10 [j]Wewe ulimponda Rahabu[k]
kama mmojawapo wa
waliochinjwa;
kwa mkono wako wenye nguvu,
uliwatawanya adui zako.
11 [l]Mbingu ni zako, nayo nchi pia ni
yako,
uliuwekea ulimwengu msingi
pamoja na vyote vilivyomo.
12 [m]Uliumba kaskazini na kusini;
Tabori na Hermoni wanaliimbia
jina lako kwa furaha.
13 [n]Mkono wako umejaa uwezo;
mkono wako una nguvu,
mkono wako wa kuume
umetukuzwa.

14 [o]Haki na hukumu ndio msingi wa kiti
chako cha enzi;
upendo na uaminifu
vinakutangulia.
15 [p]Heri ni wale ambao wamejifunza
kukusifu kwa shangwe,
wanaotembea katika mwanga
wa uwepo wako, Ee BWANA.
16 [q]Wanashangilia katika jina lako
mchana kutwa,
wanafurahi katika haki yako.

---

[a]**89:1** Za 59:16; 36:5; 40:10
[b]**89:2** Za 36:5
[c]**89:3** Eze 34:23; Hes 3:5; Ebr 7:21; Mdo 2:30
[d]**89:4** 2Sam 7:12-16; Lk 1:32, 33; Mt 1:1; Isa 9:6, 7; Rum 1:3; 1Fal 9:5; 8:16; Eze 37:24, 25; Za 132:11, 12
[e]**89:5** Za 19:1; 1:5
[f]**89:6** Mwa 1:26; Kut 9:14; Za 18:31; 113:5
[g]**89:7** Ay 5:1; Za 11:1; 47:2
[h]**89:8** Isa 6:3; Za 71:19
[i]**89:9** Za 65:7; Ay 38:11; Nah 1:4; Mt 8:26
[j]**89:10** Ay 9:13; Za 59:11; 68:1; 92:9; Isa 30:9
[k]10 Rahabu hapa ina maana jina la Misri kwa fumbo, yaani mwenye majivuno (lakini sio Rahabu wa Yos 2).
[l]**89:11** Kum 10:14; Za 24:1; 115:6; 1Nya 29:11; Mwa 1:1
[m]**89:12** Yos 19:22; Kum 3:8; 4:48; Za 98:8; Yos 12:1; Amu 4:6
[n]**89:13** Yos 4:24
[o]**89:14** Za 97:2; 85:10, 11
[p]**89:15** Za 1:1; 44:3; Hes 10:10
[q]**89:16** Za 30:4; 105:3

17 [a]Kwa kuwa wewe ni utukufu na
nguvu yao,
kwa wema wako unatukuza
pembe[b] yetu.
18 [c]Naam, ngao yetu ni mali ya BWANA,
na mfalme wetu mali ya Aliye
Mtakatifu wa Israeli.

19 Ulizungumza wakati fulani katika
maono,
kwa watu wako waaminifu,
ukasema:
"Nimeweka nguvu kwa shujaa,
nimemwinua kijana miongoni
mwa watu.
20 [d]Nimemwona Daudi, mtumishi
wangu,
na nimemtia mafuta yangu
matakatifu.
21 [e]Kitanga changu kitamtegemeza,
hakika mkono wangu utamtia
nguvu.
22 [f]Hakuna adui atakayemtoza ushuru,
hakuna mtu mwovu
atakayemwonea.
23 [g]Nitawaponda adui zake mbele zake
na kuwaangamiza watesi wake.
24 [h]Upendo wangu mkamilifu utakuwa
pamoja naye,
kwa Jina langu pembe yake
itatukuzwa.
25 [i]Nitauweka mkono wake juu ya
bahari,
mkono wake wa kuume juu ya
mito.
26 [j]Naye ataniita kwa sauti, 'Wewe ni
Baba yangu,
Mungu wangu, Mwamba na
Mwokozi wangu.'
27 [k]Nitamteua pia awe mzaliwa wangu
wa kwanza,
aliyetukuka kuliko wafalme wote
wa dunia.
28 [l]Nitadumisha upendo wangu kwake
milele,
na agano langu naye litakuwa
imara.
29 [m]Nitaudumisha uzao wake milele,
kiti chake cha enzi kama mbingu
zinavyodumu.

30 [n]"Kama wanae wataacha amri yangu
na wasifuate sheria zangu,
31 kama wakihalifu maagizo yangu
na kutoshika amri zangu,
32 [o]nitaadhibu dhambi yao kwa fimbo,
uovu wao kwa kuwapiga,
33 [p]lakini sitauondoa upendo wangu
kwake,
wala sitausaliti uaminifu wangu
kamwe.
34 [q]Mimi sitavunja agano langu
wala sitabadili lile ambalo
midomo yangu imelitamka.
35 [r]Mara moja na kwa milele, nimeapa
kwa utakatifu wangu,
nami sitamdanganya Daudi:
36 [s]kwamba uzao wake utaendelea
milele,
na kiti chake cha enzi kitadumu
mbele zangu kama jua;

---

[a] **89:17** Za 18:1, 24; 75:10; 92:10; 112:9; 148:14
[b] 17 Pembe inawakilisha nguvu.
[c] **89:18** Hos 13:10; Za 18:2; 47:9; Isa 16:5; 33:17, 22
[d] **89:20** Mdo 13:22; Za 78:70; Kut 29:7; 1Fal 1:39; 1Sam 2:35; 2Sam 22:51
[e] **89:21** Za 89:13; 18:35
[f] **89:22** Amu 3:15; 2Sam 7:10
[g] **89:23** Za 18:40; 2Sam 7:9
[h] **89:24** 2Sam 7:15; Za 61:7
[i] **89:25** Za 72:8
[j] **89:26** Za 62:2; Yer 3:4; 2Sam 7:14; 22:47; 1Nya 22:10; Yn 5:17; Ebr 1:5
[k] **89:27** Kol 1:18; Hes 24:7; Za 2:6, 7; Ufu 1:5; 19:16
[l] **89:28** Za 89:33-34; Isa 55:3
[m] **89:29** Isa 9:7; Yer 33:17; Dan 7:14; Kum 11:21; Za 89:4, 36
[n] **89:30** 2Sam 7:14; Yer 9:13
[o] **89:32** 2Sam 7:14
[p] **89:33** 2Sam 7:15
[q] **89:34** Hes 23:19
[r] **89:35** Za 110:4; Ebr 6:13, 17; Amo 4:2; 8:7
[s] **89:36** Za 89:4; 2Sam 7:18; Lk 1:33; Yn 12:34

37 [a]kitaimarishwa milele kama mwezi,
shahidi mwaminifu angani."

38 [b]Lakini wewe umemkataa,
umemdharau,
umemkasirikia sana mpakwa
mafuta wako.
39 [c]Umelikana agano lako na mtumishi
wako,
na umeinajisi taji yake
mavumbini.
40 [d]Umebomoa kuta zake zote,
na ngome zake zote umezifanya
kuwa magofu.
41 [e]Wote wapitao karibu
wamemnyang'anya mali zake;
amekuwa dharau kwa jirani zake.
42 [f]Umeutukuza mkono wa kuume wa
adui zake,
umewafanya watesi wake wote
washangilie.
43 [g]Umegeuza makali ya upanga wake,
na hukumpa msaada katika vita.
44 Umeikomesha fahari yake,
na kukiangusha kiti chake cha
enzi.
45 [h]Umezifupisha siku za ujana wake,
umemfunika kwa vazi la aibu.

46 [i]Hata lini, Ee BWANA? Utajificha
milele?
Ghadhabu yako itawaka kama
moto hata lini?
47 [j]Kumbuka jinsi maisha yangu
yanavyopita haraka.
Ni kwa ubatili kiasi gani
umemuumba mwanadamu!
48 [k]Ni mtu gani awezaye kuishi na
asione kifo,
au kujiokoa mwenyewe kutoka
nguvu za kaburi?[l]

49 [m]Ee BWANA, uko wapi upendo wako
mkuu wa mwanzoni,
ambao katika uaminifu wako
ulimwapia Daudi?
50 [n]Bwana kumbuka jinsi mtumishi
wako amesimangwa,
jinsi ninavyovumilia moyoni
mwangu dhihaka za mataifa
yote,
51 [o]dhihaka ambazo kwazo adui zako
wamenisimanga, Ee BWANA,
ambazo kwazo wamesimanga
kila hatua ya mpakwa mafuta
wako.

52 [p]Msifuni BWANA milele!
Amen na Amen.

## KITABU CHA NNE

*(Zaburi 90–106)*

### Zaburi 90

*Umilele Wa Mungu Na Udhaifu Wa Mwanadamu*

*Maombi ya Mose, mtu wa Mungu.*

1 [q]BWANA, wewe umekuwa makao
yetu
katika vizazi vyote.
2 [r]Kabla ya kuzaliwa milima
au hujaumba dunia na ulimwengu,
wewe ni Mungu tangu milele hata
milele.

---

[a]**89:37** Yer 31:35; 33:20, 21
[b]**89:38** 1Nya 28:9; Isa 22:5; Mao 2:2
[c]**89:39** Mao 5:16
[d]**89:40** Za 80:12; Isa 22:5; Mao 2:2
[e]**89:41** Amu 2:14; Za 44:13
[f]**89:42** Za 13:2; 80:6
[g]**89:43** Za 44:10
[h]**89:45** Za 39:5; 44:15; 109:29
[i]**89:46** Za 79:5
[j]**89:47** Mwa 47:9; Ay 7:7; Za 39:5; 1Pet 1:24
[k]**89:48** Mwa 5:24; Za 22:29; Ebr 11:5
[l]48 Kaburi hapa maana yake ni Kuzimu, kwa Kiebrania ni Sheol.
[m]**89:49** 2Sam 7:12; Isa 55:13
[n]**89:50** Za 69:19
[o]**89:51** Za 74:10
[p]**89:52** Za 41:13; 72:19
[q]**90:1** Kum 33:27; Efe 2:22; Ufu 21:3
[r]**90:2** Ay 38:4, 5; 10:5; 15:7; Mwa 21:33; Isa 9:6; 57:15; Za 102:24-27; Mit 8:23-26

3 [a]Huwarudisha watu mavumbini,
ukisema, "Rudini mavumbini, enyi wanadamu."
4 [b]Kwa maana kwako miaka elfu
ni kama siku moja iliyokwisha pita,
au kama kesha la usiku.
5 [c]Unawatowesha wanadamu katika usingizi wa kifo,
nao ni kama majani machanga ya asubuhi:
6 [d]ingawa asubuhi yanachipua,
ifikapo jioni huwa yamenyauka na kukauka.

7 Tumeangamizwa kwa hasira yako
na tumetishwa kwa ghadhabu yako.
8 [e]Umeyaweka maovu yetu mbele yako,
dhambi zetu za siri katika nuru ya uwepo wako.
9 [f]Tumeishi siku zetu zote chini ya ghadhabu yako,
tunamaliza miaka yetu kwa kuomboleza.
10 [g]Siku zetu za kuishi ni miaka sabini,
au miaka themanini ikiwa tuna nguvu,
lakini yote ni ya shida na taabu,
nazo zapita haraka, nasi twatoweka.

11 [h]Ni nani ajuaye nguvu za hasira yako?
Kwa maana ghadhabu yako ni kubwa
kama hofu tunayopaswa kuwa nayo kwako.

12 [i]Tufundishe kuzihesabu siku zetu vizuri,
ili tujipatie moyo wa hekima.

13 [j]Ee BWANA, uwe na huruma! Utakawia hata lini?
Wahurumie watumishi wako.
14 [k]Tushibishe asubuhi kwa upendo wako usiokoma,
ili tuweze kuimba kwa shangwe na kufurahi siku zetu zote.
15 Utufurahishe kulingana na siku ulizotuadhibu,
kulingana na miaka tuliyotaabika.
16 [l]Matendo yako na yaonekane kwa watumishi wako,
utukufu wako kwa watoto wao.

17 [m]Wema wa BWANA Mungu wetu uwe juu yetu;
uzithibitishe kazi za mikono yetu:
naam, uzithibitishe kazi za mikono yetu.

## Zaburi 91

*Mungu Mlinzi Wetu*

1 [n]Yeye akaaye mahali pa salama pake Yeye Aliye Juu Sana,
atadumu katika uvuli wake Mwenyezi.[o]
2 [p]Nitasema kumhusu BWANA, "Yeye ndiye kimbilio langu na ngome yangu,
Mungu wangu, ambaye ninamtumaini."

3 [q]Hakika yeye ataniokoa na mtego wa mwindaji,
na maradhi ya kuambukiza ya kuua.

---

[a]**90:3** Mwa 2:7; 3:9; Ay 7:21; 34:15; 1Kor 15:47; Mhu 12:7
[b]**90:4** Ebr 13:8; 2Pet 3:8; Ay 10:5
[c]**90:5** Mwa 19:15; Isa 40:6
[d]**90:6** Isa 40:6-8; Ay 14:2; Za 92:7
[e]**90:8** 2Kor 4:2; Efe 5:12; Ebr 4:13; 4:12, 13; Za 19:12; 50:21; Yer 16:17; Mit 5:21; Mhu 12:14; Rum 2:16; 1Kor 4:5
[f]**90:9** Za 78:33
[g]**90:10** Isa 23:15, 17; 2Sam 19:35; Ay 5:7; 20:8; 34:15; Yer 25:11
[h]**90:11** Za 7:11; 76:7
[i]**90:12** Za 39:4; 139:16; Mit 16:9; 20:24; Kum 32:29
[j]**90:13** Za 6:3; Kum 32:36
[k]**90:14** Za 103:5; 107:9; 145:16, 19; 31:7; 77:8; 143:8
[l]**90:16** Za 44:1; Hab 3:2
[m]**90:17** Isa 26:12; 2The 2:16, 17
[n]**91:1** Kut 33:2; Isa 49:2; Mao 4:20; Za 63:7
[o]1 Mwenyezi hapa ina maana ya Shaddai kwa Kiebrania.
[p]**91:2** Za 9:9; 91:9; 2Sam 22:2, 3
[q]**91:3** Za 124:7; Mit 6:5; 1Fal 8:37

[4] [a]Atakufunika kwa manyoya yake,
chini ya mbawa zake utapata kimbilio,
uaminifu wake utakuwa ngao na kinga yako.
[5] [b]Hutaogopa vitisho vya usiku,
wala mshale urukao mchana,
[6] wala maradhi ya kuambukiza yanayonyemelea gizani,
wala tauni iharibuyo adhuhuri.
[7] Ijapo watu elfu wataangukia kando yako,
kumi elfu mkono wako wa kuume,
lakini haitakukaribia wewe.
[8] [c]Utatazama tu kwa macho yako
na kuona adhabu ya waovu.

[9] Kama ukimfanya Aliye Juu Sana kuwa makao yako:
naam, BWANA ambaye ni kimbilio langu,
[10] [d]basi hakuna madhara yatakayokupata wewe,
hakuna maafa yataikaribia hema yako.
[11] [e]Kwa kuwa atawaagiza malaika zake kwa ajili yako,
wakulinde katika njia zako zote.
[12] [f]Mikononi mwao watakuinua,
ili usijikwae mguu wako kwenye jiwe.
[13] [g]Utawakanyaga simba na nyoka wakali,
simba mkubwa na nyoka utawaponda kwa miguu.

[14] [h]BWANA asema, "Kwa kuwa ananipenda, nitamwokoa;
nitamlinda, kwa kuwa analikiri Jina langu.
[15] [i]Ataniita, nami nitamjibu;
nitakuwa pamoja naye katika taabu,
nitamwokoa na kumheshimu.
[16] [j]Kwa siku nyingi nitamshibisha
na kumwonyesha wokovu wangu."

## Zaburi 92

*Wimbo Wa Kumsifu Mungu*

*Zaburi. Wimbo wa siku ya Sabato.*

[1] [k]Ni vyema kumshukuru BWANA
na kuliimbia jina lako, Ee Uliye Juu Sana,
[2] [l]kuutangaza upendo wako asubuhi,
na uaminifu wako wakati wa usiku,
[3] [m]kwa zeze yenye nyuzi kumi
na kwa sauti ya kinubi.

[4] [n]Ee BWANA, kwa kuwa matendo yako yamenifurahisha,
nitaziimba kwa shangwe kazi za mikono yako.
[5] [o]Ee BWANA, tazama jinsi yalivyo makuu matendo yako,
tazama jinsi yalivyo ya kina mawazo yako!
[6] [p]Mjinga hafahamu,
mpumbavu haelewi,
[7] [q]ingawa waovu huchipua kama majani
na wote watendao mabaya wanastawi,
wataangamizwa milele.

[8] Bali wewe, Ee BWANA,
utatukuzwa milele.

---

[a]**91:4** Za 61:4; 17:8; 35:2; Rum 2:12; Kum 32:10; Isa 27:3; 31:5; Zek 12:8
[b]**91:5** Ay 5:21; 5:19; Mit 3:23; Isa 43:2
[c]**91:8** Za 37:34; 58:10; Mal 1:5
[d]**91:10** Mit 1:33; 12:21; 2The 3:3; 2Pet 2:9
[e]**91:11** Mwa 32:1; Ebr 1:14; Lk 4:10; Za 34:7; Mt 4:6
[f]**91:12** Lk 1:10, 11; Ay 5:23; Mt 4:6; Za 37:24
[g]**91:13** Dan 6:22; Lk 10:19
[h]**91:14** 1Sam 2:30; Yn 12:26; Ay 22:27; Za 18:3; Yer 33:3; Zek 13:9; Ebr 5:7
[i]**91:15** Za 43:2; 1Sam 2:30
[j]**91:16** Kum 6:2; Za 21:4; 50:23
[k]**92:1** Za 27:6; 147:1; 135:3
[l]**92:2** Za 55:17
[m]**92:3** Za 71:22; 1Sam 10:5; Neh 12:27; Za 33:2; 81:2
[n]**92:4** Za 5:11; 27:6; 8:6; 111:7; 143:5
[o]**92:5** Ay 36:24; Ufu 15:3; Za 40:5; 139:17; Isa 28:29; 31:2; Rum 11:33
[p]**92:6** Za 73:22
[q]**92:7** Ay 21:7; Yer 12:1; Mal 3:15; Za 37:1

[9] [a]Ee BWANA, hakika adui zako,
hakika adui zako wataangamia.
Wote watendao mabaya
watatawanyika.
[10] [b]Umeitukuza pembe[c] yangu kama ile
ya nyati dume,
mafuta mazuri yamemiminwa juu
yangu.
[11] [d]Macho yangu yamewaona adui
zangu wakishindwa,
masikio yangu yamesikia
maangamizi ya adui zangu
waovu.

[12] [e]Wenye haki watastawi kama
mtende,
watakuwa kama mwerezi wa
Lebanoni,
[13] [f]waliopandwa katika nyumba ya
BWANA,
watastawi katika nyua za Mungu
wetu.
[14] [g]Wakati wa uzee watakuwa bado
wanazaa matunda,
watakuwa wabichi tena wamejaa
nguvu,
[15] [h]wakitangaza, "BWANA ni mkamilifu;
yeye ni Mwamba wangu,
na ndani yake hamna uovu."

## Zaburi 93

*Mungu Mfalme*

[1] [i]BWANA anatawala, amejivika
utukufu;
BWANA amejivika utukufu
tena amejivika nguvu.
Dunia imewekwa imara,
haitaondoshwa.
[2] [j]Kiti chako cha enzi kimekuwa
thabiti tangu zamani;
wewe umekuwako tangu milele.

[3] [k]Bahari zimeinua, Ee BWANA,
bahari zimeinua sauti zake;
bahari zimeinua sauti za mawimbi
yake.
[4] [l]Yeye ni mkuu kuliko ngurumo ya
maji makuu,
ni mkuu kuliko mawimbi ya
bahari:
BWANA aishiye juu sana ni mkuu.

[5] [m]Ee BWANA, sheria zako ni imara;
utakatifu umepamba nyumba yako
pasipo mwisho.

## Zaburi 94

*Mungu Mlipiza Kisasi Kwa Ajili Ya Wenye Haki*

[1] [n]Ee BWANA, ulipizaye kisasi,
Ee Mungu ulipizaye kisasi,
uangaze sasa.
[2] [o]Ee Mhukumu wa dunia, inuka,
uwalipize wenye kiburi kama
wanavyostahili.
[3] [p]Hata lini, waovu, Ee BWANA,
hata lini waovu watashangilia?

[4] [q]Wanamimina maneno ya kiburi,
watenda mabaya wote wamejaa
majivuno.
[5] [r]Ee BWANA, wanawaponda watu
wako,
wanawaonea urithi wako.
[6] [s]Wanamchinja mjane na mgeni,
na kuwaua yatima.

---

[a]**92:9** Za 45:5; 68:1; 89:10
[b]**92:10** Za 89:17; 29:6; 89:10
[c]10 Pembe inawakilisha nguvu.
[d]**92:11** Za 54:7; 91:8
[e]**92:12** Za 72:7; 1:3; 52:8; Yer 17:8; Hos 14:6; Wim 7:7
[f]**92:13** Isa 60:21; Mt 15:13; Yn 15:2, 5; Za 135:2
[g]**92:14** Za 1:3; Yn 15:2
[h]**92:15** Ay 34:10
[i]**93:1** 1Nya 16:30, 31; Za 21:5; 65:6; 24:2; 78:69; 97:1; 119:90; 104:1; 96:10; Ay 40:10; Ufu 19:6; Isa 52:7; 59:17
[j]**93:2** Mit 8:22; 2Sam 7:16; Mwa 21:33
[k]**93:3** Isa 17:12, 13; 5:30; Yer 6:23; Za 96:11; 98:7; 107:25, 29; 46:3; Ay 9:8; Isa 51:15; Yer 31:35; Hab 3:10
[l]**93:4** Za 29:10; 65:7; Yer 6:23; 18:4; Yon 1:15; Neh 9:32; Ay 9:4
[m]**93:5** Za 29:2; 5:7; 23:6
[n]**94:1** Mwa 4:24; Za 80:1; Rum 12:19; Kum 33:2
[o]**94:2** Mwa 18:25; Yak 5:9; Hes 10:35; Za 31:23
[p]**94:3** Za 13:2; Mwa 20:3
[q]**94:4** Yer 43:2; Za 52:1; Yud 15
[r]**94:5** Za 28:9; 44:2; 74:8; Isa 3:15; Yer 8:21
[s]**94:6** Kum 10:18; 20:19; Isa 1:17

7 [a]Nao husema, “BWANA haoni,
Mungu wa Yakobo hafahamu.”

8 [b]Sikizeni, enyi wajinga miongoni
mwa watu;
enyi wapumbavu, lini mtakuwa na
hekima?
9 [c]Je, aliyeweka sikio asisikie?
Aliyeumba jicho asione?
10 [d]Je, anayeadhibisha mataifa
asiadhibu?
Je, awafundishaye wanadamu
asiwe na maarifa?
11 [e]BWANA anajua mawazo ya
mwanadamu;
anajua kwamba ni ubatili.

12 [f]Ee BWANA, heri mtu
anayeadhibishwa na wewe,
mtu unayemfundisha kwa sheria
yako,
13 [g]unampa utulivu siku za shida,
mpaka shimo litakapokuwa
limechimbwa
kwa ajili ya mwovu.
14 [h]Kwa kuwa BWANA hatawakataa
watu wake,
hatauacha urithi wake.
15 [i]Hukumu itasimamishwa tena
kwenye haki,
wote walio na mioyo minyofu
wataifuata.

16 [j]Ni nani atakayeinuka dhidi ya
mwovu kwa ajili yangu?
Ni nani atakayenikinga dhidi ya
watenda maovu?
17 [k]Kama BWANA asingelinisaidia upesi,
ningelikuwa ninaishi katika
ukimya wa kifo.
18 [l]Niliposema, “Mguu wangu
unateleza,”
Ee BWANA, upendo wako
ulinishikilia.
19 [m]Wakati wasiwasi ulipokuwa mwingi
ndani yangu,
faraja yako ilinipa furaha nafsini
mwangu.

20 [n]Je, kiti cha utawala wa udhalimu
kitajiunga nawe,
ule utawala uletao taabu kutokana
na sheria zake?
21 [o]Huungana kuwashambulia wenye
haki,
kuwahukumu kufa wasio na hatia.
22 [p]Lakini BWANA amekuwa ngome
yangu,
na Mungu wangu amekuwa
mwamba ninaoukimbilia.
23 [q]Yeye atawalipa kwa ajili ya dhambi
zao
na atawaangamiza kwa ajili ya
maovu yao;
BWANA Mungu wetu
atawaangamiza.

## Zaburi 95

*Wimbo Wa Kumsifu Mungu*

1 [r]Njooni, tumwimbie BWANA kwa
furaha;
tumfanyie kelele za shangwe
Mwamba wa wokovu wetu.

---

[a]**94:7** Ay 22:14; Mwa 24:12
[b]**94:8** Kum 32:6; Za 73:22
[c]**94:9** Kut 4:11; Mit 20:12
[d]**94:10** Za 39:11; Ay 35:11; Yn 6:45; Isa 2:3; 28:26; Kut 35:34
[e]**94:11** Za 139:2; Mt 15:26; 9:4; 1Kor 3:20; 1:21
[f]**94:12** Ay 5:17; Kum 8:3; 1Kor 11:32; Mit 3:11; Ebr 12:5; 1Sam 12:23
[g]**94:13** Za 86:7; 7:15; 55:23
[h]**94:14** Kum 31:6; Za 37:28; Rum 11:2; 1Sam 12:22; 1Fal 6:13; Yer 31:37
[i]**94:15** Za 97:2; 7:10; 11:2; 36:10
[j]**94:16** Hes 10:35; Isa 14:22; Za 17:13; 59:2
[k]**94:17** Za 124:2; 31:17
[l]**94:18** Kum 32:35; Ay 12:5
[m]**94:19** Mhu 11:10; Ay 6:10
[n]**94:20** Za 58:2; Isa 10:1; 2Kor 6:14; Amo 6:3; Yer 22:30; 36:30
[o]**94:21** Za 56:6; 106:38; Mit 17:15, 26; 28:21; Isa 5:20, 23; Mt 27:1, 4; Mwa 18:23; Mit 17:15; Kut 23:7
[p]**94:22** Za 18:2; 61:2; 2Sam 22:3
[q]**94:23** Za 37:38; 145:20; 54:5; 9:5; Mit 2:22; Kut 32:34
[r]**95:1** Za 34:11; 80:2; 5:11; 81:1; Isa 44:23; Sef 3:14; 2Sam 22:47

2 [a]Tuje mbele zake kwa shukrani,
tumtukuze kwa vinanda na nyimbo.

3 [b]Kwa kuwa BWANA ni Mungu mkuu,
mfalme mkuu juu ya miungu yote.
4 [c]Mkononi mwake mna vilindi vya dunia,
na vilele vya milima ni mali yake.
5 [d]Bahari ni yake, kwani ndiye aliifanya,
na mikono yake iliumba nchi kavu.

6 [e]Njooni, tusujudu, tumwabudu,
tupige magoti mbele za BWANA Muumba wetu,
7 [f]kwa maana yeye ndiye Mungu wetu,
na sisi ni watu wa malisho yake,
kondoo chini ya utunzaji wake.

Kama mkiisikia sauti yake leo,
8 [g]msiifanye mioyo yenu migumu
kama mlivyofanya kule Meriba,[h]
kama mlivyofanya siku ile
kule Masa[i] jangwani,
9 [j]ambapo baba zenu walinijaribu na kunipima,
ingawa walikuwa wameyaona matendo yangu.
10 [k]Kwa miaka arobaini nilikasirikia kizazi kile,
nikasema, "Hawa ni taifa ambalo mioyo yao imepotoka,
nao hawajazijua njia zangu."
11 [l]Hivyo nikatangaza kwa kiapo katika hasira yangu,
"Kamwe hawataingia rahani mwangu."

## Zaburi 96

*Mungu Mfalme Mkuu*

**(1 Nyakati 16:23-33)**

1 [m]Mwimbieni BWANA wimbo mpya;
mwimbieni BWANA dunia yote.
2 [n]Mwimbieni BWANA, lisifuni jina lake;
tangazeni wokovu wake siku baada ya siku.
3 [o]Tangazeni utukufu wake katikati ya mataifa,
matendo yake ya ajabu miongoni mwa mataifa yote.

4 [p]Kwa kuwa BWANA ni mkuu mwenye kustahili kusifiwa kuliko wote;
yeye ni wa kuogopwa kuliko miungu yote.
5 [q]Kwa maana miungu yote ya mataifa ni sanamu,
lakini BWANA aliziumba mbingu.
6 [r]Fahari na enzi viko mbele yake;
nguvu na utukufu vimo patakatifu pake.

---

[a]**95:2** Za 42:4; 81:2; 100:2; Mik 6:6; Efe 5:19
[b]**95:3** Za 48:1; 86:10; 145:3; 147:5; 47:2; 96:4; 97:9
[c]**95:4** Za 63:9
[d]**95:5** Mwa 1:9; Za 146:6
[e]**95:6** Flp 2:10; Efe 3:14; 2Nya 6:13; 1Kor 6:20; 2Sam 12:16; Za 22:29; 100:3; 149:2; Lk 22:41; Isa 17:7; 54:5; Dan 6:10, 11; Ezr 9:5; 1Fal 8:54; Hos 8:14; Yn 1:3; Ay 35:10
[f]**95:7** Za 74:1; Ebr 3:7
[g]**95:8** Hes 14:22; Mk 10:5; Kut 17:7; Kum 33:8; Ebr 4:7; 3:8, 15; Za 78:40
[h]8 Meriba maana yake ni Kugombana.
[i]8 Masa maana yake ni Kujaribiwa.
[j]**95:9** Hes 14:22; 1Kor 10:9
[k]**95:10** Hes 14:34; Mdo 7:36; Isa 53:6; Ebr 3:10, 17; Za 119:67, 176; 58:3; Kut 16:35; Mit 12:26; 16:29; Yer 31:19; 50:6; Eze 34:6; Kum 8:6
[l]**95:11** Hes 14:23; Kum 1:35; Ebr 4:3; 3:7-11
[m]**96:1** Za 30:4; 33:3; 40:4; 98:1; 144:9; Isa 42:10; Ufu 5:9
[n]**96:2** Isa 42:10; Ufu 5:9; Za 68:4; 27:1; 71:15
[o]**96:3** Za 8:1; 71:17; 15:3
[p]**96:4** Za 48:1; 89:7; 95:3; Kum 28:58; 1Nya 16:25
[q]**96:5** Mwa 1:1; Isa 42:5; 41:24; Law 19:4; Yer 10:11; 2Nya 2:12; Hab 2:18-20; Mdo 19:26; 1Kor 8:4, 5
[r]**96:6** Za 21:5; 29:1; 89:17

7 [a]Mpeni BWANA, enyi jamaa za
mataifa,
mpeni BWANA utukufu na nguvu.
8 [b]Mpeni BWANA utukufu unaostahili
jina lake;
leteni sadaka na mje katika nyua
zake.
9 [c]Mwabuduni BWANA katika uzuri wa
utakatifu wake;
dunia yote na itetemeke mbele
zake.

10 [d]Katikati ya mataifa semeni, "BWANA
anatawala."
Ulimwengu ameuweka imara,
hauwezi kusogezwa;
atawahukumu watu kwa uadilifu.
11 [e]Mbingu na zishangilie, nchi na
ifurahi;
bahari na ivume, na vyote
vilivyomo ndani yake;
12 [f]mashamba na yashangilie,
pamoja na vyote vilivyomo ndani
yake.
Kisha miti yote ya msituni itaimba
kwa furaha;
13 [g]itaimba mbele za BWANA kwa
maana anakuja,
anakuja kuihukumu dunia.
Ataihukumu dunia kwa haki,
na mataifa katika kweli yake.

## Zaburi 97

*Mungu Mtawala Mkuu*

1 [h]BWANA anatawala, nchi na ifurahi,
visiwa vyote vishangilie.
2 [i]Mawingu na giza nene
vinamzunguka,
haki na hukumu ndio msingi wa
kiti chake cha enzi.
3 [j]Moto hutangulia mbele zake
na huteketeza adui zake pande
zote.
4 [k]Umeme wake wa radi humulika
dunia,
nchi huona na kutetemeka.
5 [l]Milima huyeyuka kama nta mbele
za BWANA,
mbele za Bwana wa dunia yote.
6 [m]Mbingu zinatangaza haki yake,
na mataifa yote huona utukufu
wake.

7 [n]Wote waabuduo sanamu
waaibishwa,
wale wajisifiao sanamu:
mwabuduni yeye, enyi miungu
yote!

8 [o]Sayuni husikia na kushangilia,
vijiji vya Yuda vinafurahi
kwa sababu ya hukumu zako, Ee
BWANA.
9 [p]Kwa kuwa wewe, Ee BWANA, ndiwe
Uliye Juu Sana kuliko dunia
yote;
umetukuka sana juu ya miungu
yote.

---

[a]**96:7** Za 29:1; 22:27
[b]**96:8** Za 45:12; 51:19; 72:10; 65:4; 84:10; 92:13; 100:4
[c]**96:9** Kut 15:14; 23:25; Yon 1:9; Za 93:5; 114:7; 33:8
[d]**96:10** Za 97:1; 24:2; 78:69; 119:90; 93:1; 58:11; 67:4; 98:9
[e]**96:11** Ufu 12:12; Za 97:1; Isa 49:13
[f]**96:12** Isa 44:23; 55:12; Eze 17:24; Za 65:13
[g]**96:13** Ufu 19:11; Za 7:11; Mdo 17:31; Za 86:11
[h]**97:1** Kut 15:18; Za 93:1; 96:10; 99:1; 96:11; Isa 24:23; 52:7
[i]**97:2** Ay 22:14; Kut 19:9; Za 89:14
[j]**97:3** Dan 7:10; Hab 3:5; Isa 9:19; Yoe 1:19; 2:3; Hab 3:5; 2Sam 22:9
[k]**97:4** Ay 36:30; 2Sam 22:8; Za 18:7; 104:32; Ufu 6:12
[l]**97:5** Za 46:2, 6; 22:14; Yos 3:11
[m]**97:6** Za 50:6; 98:2; 19:1
[n]**97:7** Kut 12:12; 20:4; Isa 37:18, 19; 42:17; Law 26:1; Kum 5:8; Yer 10:14; Ebr 1:6; Za 16:4
[o]**97:8** Za 9:2; 48:11
[p]**97:9** Ay 34:29; Efe 1:21; Za 7:8; 47:9

[10] [a]Wale wanaompenda BWANA na
wauchukie uovu,
kwa maana yeye hulinda maisha
ya waaminifu wake
na kuwaokoa kutoka mkononi
mwa mwovu.
[11] [b]Nuru huangaza wenye haki
na furaha kwa watu wanyofu wa
moyo.
[12] [c]Furahini katika BWANA, ninyi mlio
wenye haki,
lisifuni jina lake takatifu.

## Zaburi 98

*Mungu Mtawala Wa Dunia*

*Zaburi.*

[1] [d]Mwimbieni BWANA wimbo mpya,
kwa maana ametenda mambo ya
ajabu;
kitanga chake cha kuume na mkono
wake mtakatifu
umemfanyia wokovu.
[2] [e]BWANA ameufanya wokovu wake
ujulikane
na amedhihirisha haki yake kwa
mataifa.
[3] [f]Ameukumbuka upendo wake
na uaminifu wake kwa nyumba ya
Israeli;
miisho yote ya dunia imeuona
wokovu wa Mungu wetu.
[4] [g]Mpigieni BWANA kelele za shangwe,
dunia yote,
ipaze sauti kwa nyimbo za
shangwe na vinanda;
[5] [h]mwimbieni BWANA kwa kinubi,
kwa kinubi na sauti za kuimba,
[6] [i]kwa tarumbeta na mvumo wa
baragumu za pembe za
kondoo dume:
shangilieni kwa furaha mbele za
BWANA, aliye Mfalme.

[7] [j]Bahari na ivume na kila kiliomo
ndani yake,
dunia na wote wakaao ndani yake.
[8] [k]Mito na ipige makofi,
milima na iimbe pamoja kwa
furaha,
[9] [l]vyote na viimbe mbele za BWANA,
kwa maana yuaja kuhukumu
dunia.
Atahukumu dunia kwa haki
na mataifa kwa haki.

## Zaburi 99

*Mungu Mfalme Mkuu*

[1] [m]BWANA anatawala,
mataifa na yatetemeke;
anakalia kiti cha enzi katikati ya
makerubi,
dunia na itikisike.
[2] [n]BWANA ni mkuu katika Sayuni;
ametukuzwa juu ya mataifa yote.
[3] [o]Wanalisifu jina lako ambalo ni kuu
na la kuogopwa:
yeye ni mtakatifu!

---

[a]**97:10** Ay 28:28; Mit 2:8; Za 145:20; 31:23; 101:3; 37:28, 40; 34:7; Yer 15:21; 20:13; Dan 3:28; 6:16; 1Sam 2:9; Rum 12:9; 7:15; Amo 5:15
[b]**97:11** Ay 22:28; Za 11:5; 7:10
[c]**97:12** Ay 22:19; Flp 4:4; Kut 3:15; Isa 41:16; Za 99:5; 104:34
[d]**98:1** Za 30:4; 96:1, 3; 44:3; Kut 15:1, 6; Lk 1:51; Yos 4:24; Ay 40:9; Isa 52:10; 53:1; 63:5; 12:5; 51:9; 59:16
[e]**98:2** Za 67:2; Lk 2:30; 3:6; Rum 3:25; Isa 52:10; 62:2
[f]**98:3** 1Nya 16:15; Mwa 49:10; Za 48:10; 50:23; Kum 4:31; Mik 7:20; Isa 49:6; Lk 1:54; 3:6; Mdo 13:47
[g]**98:4** Za 20:5; Isa 12:6; 44:23; 52:9; 54:1; 55:12
[h]**98:5** Za 33:2; 92:3; 147:7; Isa 51:3
[i]**98:6** Hes 10:2; 10:10; 2Sam 6:15; Kut 19:13; Isa 12:6; Za 2:6; 47:7; 20:5; 100:1; 1Nya 15:28; 2Nya 29:27
[j]**98:7** Za 93:3; 24:1
[k]**98:8** 2Fal 11:12; Za 148:9; 44:23
[l]**98:9** Za 96:10
[m]**99:1** 1Nya 16:30, 31; Za 97:1; 2Sam 6:2; Kut 15:14; 25:22
[n]**99:2** Za 48:1; 148:13; 2:6; 46:10; 97:9; 113:4; Kut 15:1
[o]**99:3** Za 103:1; 33:21; 97:12; 76:1; 30:4; 106:47; 111:9; 145:21; 148:5; Kut 15:11

4 [a]Mfalme ni mwenye nguvu na
hupenda haki,
wewe umethibitisha adili;
katika Yakobo umefanya
yaliyo haki na sawa.
5 [b]Mtukuzeni BWANA Mungu wetu,
na mkaabudu katika mahali pa
kuwekea miguu yake;
yeye ni mtakatifu.

6 [c]Mose na Aroni walikuwa miongoni
mwa makuhani wake,
Samweli alikuwa miongoni mwa
walioliitia jina lake;
walimwita BWANA,
naye aliwajibu.
7 [d]Alizungumza nao kutoka nguzo ya
wingu;
walizishika sheria zake na amri
alizowapa.

8 [e]Ee BWANA, wetu,
ndiwe uliyewajibu,
kwa Israeli ulikuwa Mungu mwenye
kusamehe,
ingawa uliadhibu matendo yao
mabaya.
9 Mtukuzeni BWANA Mungu wetu,
mwabuduni kwenye mlima wake
mtakatifu,
kwa maana BWANA Mungu wetu
ni mtakatifu.

## Zaburi 100

*Dunia Yote Yaitwa Kumsifu Mungu*

*Zaburi ya shukrani.*

1 [f]Mpigieni BWANA kelele za shangwe,
dunia yote.
2 [g]Mwabuduni BWANA kwa furaha;
njooni mbele zake kwa nyimbo za
shangwe.
3 [h]Jueni kwamba BWANA ndiye
Mungu.
Yeye ndiye alituumba, sisi tu mali
yake;
sisi tu watu wake,
kondoo wa malisho yake.

4 [i]Ingieni malangoni mwake kwa
shukrani
na katika nyua zake kwa kusifu,
mshukuruni yeye na kulisifu jina
lake.
5 [j]Kwa maana BWANA ni mwema
na upendo wake wadumu milele;
uaminifu wake unadumu kwa
vizazi vyote.

## Zaburi 101

*Ahadi Ya Kuishi Kwa Uadilifu Na Kwa Haki*

*Zaburi ya Daudi.*

1 [k]Nitaimba juu ya upendo wako na
haki yako;
kwako wewe, Ee BWANA, nitaimba
sifa.
2 [l]Nitazingatia kuishi maisha yasiyo na
lawama:
utakuja kwangu lini?

Nitatembea nyumbani mwangu
kwa moyo usio na lawama.
3 [m]Sitaweka mbele ya macho yangu
kitu kiovu.

Ninayachukia matendo ya watu
wasio na imani;
hawatashikamana nami.
4 [n]Moyo wa ukaidi utakuwa mbali
nami;
nitajitenga na kila ubaya.

---

[a]**99:4** 1Fal 10:9; Za 98:9; Mwa 18:19, 25; Ufu 15:3; Ay 36:5; Kum 32:3, 4; Isa 11:3-5; Yer 23:5; Za 2:6
[b]**99:5** Isa 66:1; Kut 15:2; 1Nya 28:2; Za 132:7
[c]**99:6** Kut 24:6; 28:1; 1Sam 7:5; Za 4:3; 91:15
[d]**99:7** Kut 13:21; 19:9; Hes 11:25; 12:5
[e]**99:8** Hes 14:20; Sef 3:7; Kum 9:20; Kut 22:27; Law 26:18
[f]**100:1** Za 98:6
[g]**100:2** Kum 10:12; Za 95:2
[h]**100:3** 1Fal 18:21; Za 74:1; 46:10; 79:13; Isa 19:25; 63:8, 17-19; 64:9; Ay 10:3, 8, 9; Mhu 12:1; Efe 2:10; Eze 34:30
[i]**100:4** Za 42:4; 96:8; 116:17
[j]**100:5** 1Nya 16:34; Ezr 3:11; Za 106:1; 108:4; 119:90
[k]**101:1** Za 33:1; 51:14; 89:1; 145:7
[l]**101:2** Mwa 17:1; 18:10; 1Sam 18:14; Kum 6:7; Flp 1:10; 1Fal 9:4; 3:14
[m]**101:3** Yos 23:6; 1Sam 12:20; Yer 16:18; Eze 11:21; Hos 9:10; Za 5:5
[n]**101:4** Mit 3:32; 6:16-19; 11:20; Mt 7:23; 1Kor 5:11; 2Tim 2:19

5 [a]Kila amsingiziaye jirani yake kwa siri,
huyo nitamnyamazisha;
mwenye macho ya dharau na moyo wa kiburi
huyo sitamvumilia.

6 [b]Macho yangu yatawaelekea waaminifu katika nchi,
ili waweze kuishi pamoja nami;
yeye ambaye moyo wake hauna lawama
atanitumikia.

7 Mdanganyifu hatakaa
nyumbani mwangu,
yeye asemaye kwa uongo
hatasimama mbele yangu.

8 [c]Kila asubuhi nitawanyamazisha
waovu wote katika nchi;
nitamkatilia mbali kila mtenda mabaya
kutoka mji wa BWANA.

## Zaburi 102

*Maombi Ya Mtu Mwenye Taabu*

*Maombi ya mtu aliyechoka. Anapoteseka na kumimina malalamiko yake kwa BWANA.*

1 [d]Ee BWANA, usikie maombi yangu,
kilio changu cha kuomba msaada kikufikie.
2 [e]Usinifiche uso wako
ninapokuwa katika shida.
Unitegee sikio lako,
ninapoita, unijibu kwa upesi.

3 Kwa kuwa siku zangu zinatoweka kama moshi,
mifupa yangu inaungua kama kaa la moto.
4 [f]Moyo wangu umefifia na kunyauka kama jani,
ninasahau kula chakula changu.
5 [g]Kwa sababu ya kusononeka kwangu kwa uchungu,
nimebakia ngozi na mifupa.
6 [h]Nimekuwa kama bundi wa jangwani,
kama bundi kwenye magofu.
7 [i]Nilalapo sipati usingizi,
nimekuwa kama ndege mpweke
kwenye paa la nyumba.
8 [j]Mchana kutwa adui zangu hunidhihaki,
wale wanaonizunguka hutumia jina langu kama laana.
9 [k]Ninakula majivu kama chakula changu
na nimechanganya kinywaji changu na machozi
10 [l]kwa sababu ya ghadhabu yako kuu,
kwa maana umeniinua na kunitupa kando.
11 [m]Siku zangu ni kama kivuli cha jioni,
ninanyauka kama jani.

12 [n]Lakini wewe, Ee BWANA, umeketi katika kiti chako cha enzi milele,
sifa zako za ukuu zaendelea vizazi vyote.
13 [o]Utainuka na kuihurumia Sayuni,
kwa maana ni wakati wa kumwonyesha wema;
wakati uliokubalika umewadia.

---

[a]**101:5** Kut 20:16; Law 19:16; Za 10:5; Mit 6:17; Lk 18:14
[b]**101:6** Za 101:2; 119:1
[c]**101:8** Za 5:3; 75:10; 118:10-12; 46:4; Yos 21:12; 2Sam 3:39; Hos 9:2
[d]**102:1** Za 4:1; Kut 2:23
[e]**102:2** Za 22:24; 31:2; 88:2; 2Fal 19:16
[f]**102:4** Za 37:2; 90:5-6; 1Sam 1:7; Ezr 10:6; Ay 33:26
[g]**102:5** Za 6:6
[h]**102:6** Isa 34:11; Sef 2:14; Kum 14:15-17; Ay 30:29
[i]**102:7** Za 77:4; 38:11
[j]**102:8** Za 31:11; 42:10; Mdo 23:12
[k]**102:9** Isa 44:20; Za 6:6; 42:3; 80:5
[l]**102:10** Za 7:11; 38:3; 30:7
[m]**102:11** 1Nya 29:15; Ay 14:2; 8:12; Za 39:6; Yak 1:10
[n]**102:12** Kut 15:18; 3:15; Isa 55:13; 63:12; 40:2; Za 135:13
[o]**102:13** Za 119:126; 44:26; 77:7; Kum 32:36; 1Fal 3:26; Isa 54:8; 60:10; 40:2; Zek 10:6; Kut 13:10; Dan 8:19; Mdo 1:7

14 [a]Kwa maana mawe yake ni ya
thamani kwa watumishi
wako,
vumbi lake lenyewe hulionea
huruma.
15 [b]Mataifa wataogopa jina la BWANA,
wafalme wote wa dunia
watauheshimu utukufu wako.
16 [c]Kwa maana BWANA ataijenga tena
Sayuni
na kutokea katika utukufu wake.
17 [d]Ataitikia maombi ya mtu mkiwa,
wala hatadharau hoja yao.

18 [e]Hili na liandikwe kwa ajili ya kizazi
kijacho,
ili taifa litakaloumbwa baadaye
waweze kumsifu BWANA:
19 [f]"BWANA alitazama chini kutoka
patakatifu pake palipo juu,
kutoka mbinguni alitazama dunia,
20 [g]kusikiliza vilio vya uchungu vya
wafungwa
na kuwaweka huru wale
waliohukumiwa kufa."
21 [h]Kwa hiyo jina la BWANA latangazwa
huko Sayuni
na sifa zake katika Yerusalemu,
22 [i]wakati mataifa na falme
zitakapokusanyika
ili kumwabudu BWANA.

23 [j]Katika kuishi kwangu alivunja
nguvu zangu,
akafupisha siku zangu.
24 [k]Ndipo niliposema:
"Ee Mungu wangu, usinichukue
katikati ya siku zangu;
miaka yako inaendelea vizazi
vyote.
25 [l]Hapo mwanzo uliweka misingi ya
dunia,
nazo mbingu ni kazi ya mikono
yako.
26 [m]Hizi zitatoweka, lakini wewe
utadumu,
zote zitachakaa kama vazi.
Utazibadilisha kama nguo
nazo zitaondoshwa.
27 [n]Lakini wewe, U yeye yule,
nayo miaka yako haikomi kamwe.
28 [o]Watoto wa watumishi wako
wataishi mbele zako;
wazao wao wataimarishwa mbele
zako."

### Zaburi 103

*Upendo Wa Mungu*

*Zaburi ya Daudi.*

1 [p]Ee nafsi yangu, umhimidi BWANA.
Vyote vilivyomo ndani yangu
vilihimidi jina lake takatifu.
2 [q]Ee nafsi yangu, umhimidi BWANA,
wala usisahau wema wake wote,
3 [r]akusamehe dhambi zako zote,
akuponya magonjwa yako yote,
4 [s]aukomboa uhai wako na kaburi,
akuvika taji ya upendo na huruma,

---

[a]**102:14** Dan 9:2
[b]**102:15** 1Fal 8:43; Isa 2:2; Za 67:7; 76:12; 138:4; 148:11
[c]**102:16** Za 51:18; 8:1; Isa 60:1, 2
[d]**102:17** Neh 2:8; 1Fal 8:29; Za 4:1; 6:9
[e]**102:18** Rum 4:24; 15:4; Za 22:31; 1Kor 10:1; Isa 43:21
[f]**102:19** Kum 26:15; Za 14:2; 53:2
[g]**102:20** Za 68:6; Lk 4:19
[h]**102:21** Za 22:22; 9:14
[i]**102:22** Hos 1:11; Za 22:27; Isa 49:22, 23; Zek 8:20-23
[j]**102:23** Za 39:5
[k]**102:24** Mwa 21:33; Ay 36:26; Za 90:2; Hab 1:12; Ufu 1:4, 8
[l]**102:25** Mwa 1:1; Ebr 1:10; 2Nya 2:12; Za 8:3; Kut 20:11; Ay 38:4-7
[m]**102:26** Rum 8:20; Isa 51:6; 13:10, 13; 66:21; 34:4; Mt 24:35; Yoe 2:10; Eze 32:8; 2Pet 3:7-10; Ufu 20:11
[n]**102:27** Hes 23:19; Ebr 13:8; Mal 3:6; Yak 1:17; Za 9:7
[o]**102:28** Za 69:36; 25:13; 89:4
[p]**103:1** Za 28:6; 104:1; 30:4
[q]**103:2** Za 106:1; 117:1; Kum 6:12; Za 77:11
[r]**103:3** Kut 34:7; 15:26; Kol 3:13; 1Pet 2:24; 1Yn 1:9
[s]**103:4** Za 34:22; 56:13; 8:5; 23:6; Isa 43:1

5 [a]atosheleza mahitaji yako kwa vitu vyema,
ili ujana wako uhuishwe kama wa tai.

6 [b]BWANA hutenda haki,
naye huwapa hukumu ya haki wote wanaoonewa.

7 [c]Alijulisha Mose njia zake,
na wana wa Israeli matendo yake.
8 [d]BWANA ni mwingi wa huruma na mwenye neema;
si mwepesi wa hasira, bali amejaa upendo.
9 [e]Yeye hatalaumu siku zote,
wala haweki hasira yake milele,
10 [f]yeye hatutendei kulingana na dhambi zetu
wala hatupatilizi kwa kadiri ya maovu yetu.
11 [g]Kama vile mbingu zilivyo juu ya dunia sana,
ndivyo wema wake ulivyo mwingi kwa wanaomcha;
12 [h]kama mashariki ilivyo mbali na magharibi,
ndivyo Mungu alivyoziweka dhambi zetu mbali nasi.
13 [i]Kama baba alivyo na huruma kwa watoto wake,
ndivyo BWANA anavyowahurumia wale wanaomcha;
14 [j]kwa kuwa anajua tulivyoumbwa,
anakumbuka kwamba sisi tu mavumbi.
15 [k]Kuhusu mwanadamu, siku zake ni kama majani,
anachanua kama ua la shambani;
16 [l]upepo huvuma juu yake nalo hutoweka,
mahali pake hapalikumbuki tena.
17 [m]Lakini kutoka milele hata milele
upendo wa BWANA uko kwa wale wamchao,
nayo haki yake kwa watoto wa watoto wao:
18 [n]kwa wale walishikao agano lake
na kukumbuka kuyatii mausia yake.

19 BWANA ameweka imara kiti chake cha enzi mbinguni,
ufalme wake unatawala juu ya vyote.
20 [o]Mhimidini BWANA, enyi malaika zake,
ninyi mlio mashujaa mnaozitii amri zake,
ninyi mnaotii neno lake.
21 [p]Mhimidini BWANA, ninyi jeshi lake lote la mbinguni,
ninyi watumishi wake mnaofanya mapenzi yake.
22 [q]Mhimidini BWANA, kazi zake zote
kila mahali katika milki yake.

---

[a]**103:5** Ay 33:25; Za 90:14; 104:28; 119:25, 93; 2Kor 4:16; Kut 19:4
[b]**103:6** Za 9:8; 74:21; 65:5; Isa 9:7; Lk 4:10
[c]**103:7** Za 99:7; 147:19; 106:22; Kut 33:13
[d]**103:8** Kut 22:27; 34:6; Za 86:15; Mik 7:18-19; Yak 5:11; Kum 5:10; Hes 14:18
[e]**103:9** Yer 3:5, 12; Mik 7:18; Isa 57:16; Za 30:5; 79:5
[f]**103:10** Ezr 9:13; Rum 6:23
[g]**103:11** Efe 3:18; Za 13:5; 57:10; 100:5; 106:45; 117:2; Mao 3:22; 2Nya 6:31
[h]**103:12** 2Sam 12:13; Rum 4:7; Efe 1:7; 2:5; Isa 43:25
[i]**103:13** Mal 3:17; Kum 8:5; 1Yn 3:1; Isa 63:15, 16
[j]**103:14** Za 119:73; 139:13-15; 146:4; Isa 29:16; Mwa 2:7
[k]**103:15** Za 37:2; 90:5; 102:11; Yak 1:10; Isa 40:6; Ay 14:2
[l]**103:16** Isa 40:7; Hag 1:9; Ay 7:8
[m]**103:17** Mwa 48:11; Ezr 9:12; Kut 20:6
[n]**103:18** Yn 14:15; Kum 7:9; 28:9; Za 119:52; Hes 15:40; Za 47:8; 80:1; 113:5; 22:28; 66:7; Dan 4:17
[o]**103:20** Neh 9:6; Lk 2:13; Ebr 1:14; Za 29:1; 28:6; 107:25; 135:7; 148:8; Mt 6:10
[p]**103:21** 1Fal 22:19; Neh 7:73; Dan 7:9; Mwa 32:2
[q]**103:22** Za 104:1; 67:3; 19:1; 145:10; 150:1, 6

Ee nafsi yangu, umhimidi BWANA.

## Zaburi 104

*Kumsifu Muumba*

1 [a]Ee nafsi yangu, umhimidi BWANA.

Ee BWANA Mungu wangu, wewe ni
mkuu sana,
umejivika utukufu na enzi.
2 [b]Amejifunika katika nuru kama vile
kwa vazi,
amezitandaza mbingu kama hema
3 [c]na kuziweka nguzo za orofa yake
juu ya maji.
Huyafanya mawingu kuwa gari lake,
na hupanda kwenye mbawa za
upepo.
4 [d]Huzifanya pepo kuwa wajumbe[e]
wake,
miali ya moto watumishi wake.

5 [f]Ameiweka dunia kwenye misingi
yake,
haiwezi kamwe kuondoshwa.
6 [g]Uliifunika kwa kilindi kama kwa
vazi,
maji yalisimama juu ya milima.
7 [h]Lakini kwa kukemea kwako maji
yalikimbia,
kwa sauti ya radi yako yakatoroka,
8 [i]yakapanda milima, yakateremka
mabondeni,
hadi mahali pale ulipoyakusudia.
9 [j]Uliyawekea mpaka ambao hayawezi
kuuvuka,
kamwe hayataifunika dunia tena.
10 [k]Huzifanya chemchemi zimwage maji
mabondeni,
hutiririka kati ya milima.
11 [l]Huwapa maji wanyama wote wa
kondeni,
punda-mwitu huzima kiu yao.
12 [m]Ndege wa angani hufanya viota
kando ya maji,
huimba katikati ya matawi.
13 [n]Huinyeshea milima kutoka orofa
zake,
dunia inatoshelezwa kwa matunda
ya kazi yake.
14 [o]Huyafanya majani ya mifugo yaote,
na mimea kwa watu kulima,
wajipatie chakula kutoka ardhini:
15 [p]divai ya kuufurahisha moyo wa
mwanadamu,
mafuta kwa ajili ya kung'arisha
uso wake,
na mkate wa kutia mwili nguvu.
16 [q]Miti ya BWANA inanyeshewa vizuri,
mierezi ya Lebanoni aliyoipanda.
17 [r]Humo ndege hufanya viota vyao,
korongo ana nyumba yake kwenye
msunobari.
18 [s]Milima mirefu ni makao ya
mbuzi-mwitu,
majabali ni kimbilio la pelele.

19 [t]Mwezi hugawanya majira,
na jua hutambua wakati wake wa
kutua.
20 [u]Unaleta giza, kunakuwa usiku,
wanyama wote wa mwituni
huzurura.

---

[a]**104:1** Za 103:22; Ay 40:10
[b]**104:2** Yer 43:12; 51:15; 1Tim 6:16; Ay 9:8; 37:18; Isa 44:24; 49:18, 22; 42:5; 40:22; Zek 12:1; Za 18:12; 19:4
[c]**104:3** Amo 9:6; Za 18:10; 24:2; Kum 33:26; Isa 19:1; Nah 1:3; 2Fal 12:11
[d]**104:4** Za 148:8; Mwa 3:24; 2Fal 2:11; Ebr 1:7
[e]4 Au: malaika.
[f]**104:5** Kut 31:17; Ay 26:7; Za 24:1, 2; 121:2; 102:25; 1Sam 2:8
[g]**104:6** Mwa 7:19; 1:2; 2Pet 3:6
[h]**104:7** Za 18:15; 29:3; Kut 9:23
[i]**104:8** Za 33:7; Ay 38:10
[j]**104:9** Yer 5:22; Za 16:6; 33:7; Ay 26:10; Mwa 1:9; 9:11
[k]**104:10** Za 107:33; Isa 41:16
[l]**104:11** Za 104:13; Mwa 16:12; Isa 32:14; Yer 14:6
[m]**104:12** Za 104:17; Mt 8:20; 13:32
[n]**104:13** Za 135:7; 147:8; Yer 10:13
[o]**104:14** Ay 38:27; 28:5; Mwa 1:30; Za 147:8; 136:25
[p]**104:15** Mwa 14:18; Amu 9:13; Za 23:5; 92:10; Lk 7:46; Kum 8:3; Mit 31:6, 7; Yer 12:12; Mk 14:23; Mhu 10:19; Yn 2:9, 10
[q]**104:16** Mwa 1:11; Za 29:5; 72:16; Hes 24:6
[r]**104:17** Za 104:12
[s]**104:18** Mit 30:26; Kum 14:5
[t]**104:19** Mwa 1:14; Za 19:6; Ay 38:12
[u]**104:20** Isa 45:7; Amo 5:8; Za 74:16; 50:10

21 [a]Simba hunguruma kwa mawindo
yao,
na kutafuta chakula chao kutoka
kwa Mungu.
22 [b]Jua huchomoza, nao huondoka,
hurudi na kulala katika mapango
yao.
23 [c]Kisha mwanadamu huenda kazini
mwake,
katika kazi yake mpaka jioni.

24 [d]Ee BWANA, jinsi matendo yako
yalivyo mengi!
Kwa hekima ulizifanya zote,
dunia imejaa viumbe vyako.
25 [e]Pale kuna bahari, kubwa na yenye
nafasi tele,
imejaa viumbe visivyo na idadi,
vitu vyenye uhai vikubwa na
vidogo.
26 [f]Huko meli huenda na kurudi,
pia Lewiathani,[g] uliyemuumba
acheze ndani yake.

27 [h]Hawa wote wanakutazamia wewe,
uwape chakula chao kwa wakati
wake.
28 [i]Wakati unapowapa,
wanakikusanya,
unapofumbua mkono wako,
wao wanashibishwa mema.
29 [j]Unapoficha uso wako,
wanapata hofu,
unapoondoa pumzi yao,
wanakufa na kurudi mavumbini.

30 [k]Unapopeleka Roho wako,
wanaumbwa,
nawe huufanya upya uso wa
dunia.

31 [l]Utukufu wa BWANA na udumu
milele,
BWANA na azifurahie kazi zake:
32 [m]yeye aitazamaye dunia, nayo
ikatetemeka,
aigusaye milima, nayo ikatoa
moshi.

33 [n]Nitamwimbia BWANA maisha yangu
yote;
nitaimba sifa kwa Mungu wangu
muda wote ninaoishi.
34 [o]Kutafakari kwangu na kumpendeze
yeye,
ninapofurahi katika BWANA.
35 [p]Lakini wenye dhambi na watoweke
katika dunia
na waovu wasiwepo tena.

Ee nafsi yangu, msifu BWANA.

Msifuni BWANA.[q]

## Zaburi 105

*Uaminifu Wa Mungu Kwa Israeli*

**(1 Nyakati 16:8-22)**

1 [r]Mshukuruni BWANA, liitieni jina
lake,
wajulisheni mataifa yale
aliyoyatenda.
2 [s]Mwimbieni yeye, mwimbieni yeye
sifa,
waambieni matendo yake yote ya
ajabu.

[a]**104:21** Amo 3:4; Za 145:15; Mt 6:26; Yoe 1:20
[b]**104:22** Za 37:8
[c]**104:23** Mwa 3:19; Amu 19:16
[d]**104:24** Mwa 1:31; 1:20-22; Za 40:5; 24:1; 50:10, 11
[e]**104:25** Za 69:34; Eze 47:10
[f]**104:26** Za 107:23; Eze 27:9; Yon 1:3; Ay 41:1; 40:20; Mwa 1:21
[g]26 Lewiathani ni mnyama mkubwa wa baharini mwenye magamba anayefanana na joka kubwa, mwenye umbo la kutisha, asiyeweza kuvuliwa.
[h]**104:27** Ay 36:31; Za 147:9; 145:15; Rum 11:36
[i]**104:28** Isa 58:11; Za 103:5; 145:16
[j]**104:29** Kum 31:17; Ay 7:21; Mhu 12:7
[k]**104:30** Mwa 1:2; Isa 32:15
[l]**104:31** Kut 40:35; Rum 11:36; Mwa 1:4; Za 8:1
[m]**104:32** Kut 19:18; Hab 3:10; Za 97:4; 144:5
[n]**104:33** Kut 15:1; Za 108:1
[o]**104:34** Za 2:11; 9:2; 32:11
[p]**104:35** Ay 7:10; Za 28:6; 37:38; 105:45; 106:48
[q]35 Msifuni BWANA kwa Kiebrania ni Hallelu Yah.
[r]**105:1** 1Nya 16:34; Za 80:18; 99:6; 116:13; Yoe 2:32; Mdo 2:21; Isa 12:4
[s]**105:2** Za 30:4; 146:2; 33:3; 96:1; 7:17; 18:49; 27:6; 59:17; 71:22; 75:1

3 [a]Lishangilieni jina lake takatifu,
mioyo ya wale wamtafutao
BWANA na ifurahi.
4 [b]Mtafuteni BWANA na nguvu zake,
utafuteni uso wake siku zote.

5 [c]Kumbuka matendo ya ajabu
aliyoyafanya,
miujiza yake na hukumu
alizozitamka,
6 [d]enyi wazao wa Abrahamu mtumishi
wake,
enyi wana wa Yakobo, wateule
wake.
7 [e]Yeye ndiye BWANA Mungu wetu,
hukumu zake zimo duniani pote.

8 [f]Hulikumbuka agano lake milele,
neno ambalo aliamuru, kwa vizazi
elfu,
9 [g]agano alilolifanya na Abrahamu,
kiapo alichomwapia Isaki.
10 [h]Alilithibitisha kwa Yakobo kuwa
amri,
kwa Israeli liwe agano la milele:
11 [i]"Nitakupa wewe nchi ya Kanaani
kuwa sehemu utakayoirithi."

12 [j]Walipokuwa wachache kwa idadi,
wachache sana na wageni ndani
yake,
13 [k]walitangatanga kutoka taifa moja
hadi jingine,
kutoka ufalme mmoja hadi
mwingine.
14 [l]Hakuruhusu mtu yeyote awaonee;
kwa ajili yao aliwakemea
wafalme, akisema:
15 [m]"Msiwaguse niliowatia mafuta;
msiwadhuru manabii wangu."

16 [n]Akaiita njaa juu ya nchi
na kuharibu chakula chao chote,
17 [o]naye akatuma mtu mbele yao,
Yosefu, aliyeuzwa kama mtumwa.
18 [p]Walichubua miguu yake kwa
minyororo,
shingo yake ilifungwa kwa chuma,
19 [q]hadi yale aliyotangulia kusema
yalipotimia,
hadi neno la BWANA
lilipomthibitisha.
20 [r]Mfalme alituma watu wakamfungua,
mtawala wa watu alimwachia
huru.
21 Alimfanya mkuu wa nyumba yake,
mtawala juu ya vyote alivyokuwa
navyo,
22 [s]kuwaelekeza wakuu wa mfalme
apendavyo
na kuwafundisha wazee wake
hekima.

23 [t]Kisha Israeli akaingia Misri,
Yakobo akaishi kama mgeni katika
nchi ya Hamu.
24 [u]BWANA aliwafanya watu wake
kuzaana sana,
akawafanya kuwa wengi sana
kuliko adui zao,
25 [v]ndiye aliigeuza mioyo yao
iwachukie watu wake,
wakatenda hila dhidi ya
watumishi wake.

[a]**105:3** Za 89:16
[b]**105:4** Za 24:6; 27:8
[c]**105:5** Za 40:5; Kum 7:18; 8:2
[d]**105:6** Za 105:42; Kum 10:15; Za 106:5
[e]**105:7** Isa 26:8
[f]**105:8** Mwa 9:15; Za 106:45; 111:5; Eze 16:60; Lk 1:72
[g]**105:9** Mwa 22:16-18; 15:18; Ebr 6:17; Lk 1:73; 17:2; 12:7; Gal 3:15-18; Dan 9:4
[h]**105:10** Mwa 28:13-15; Isa 55:3
[i]**105:11** Mwa 12:7; Hes 34:2
[j]**105:12** Kum 7:7; Ebr 11:9; Mwa 17:8; 23:4; 34:30
[k]**105:13** Mwa 15:13-16; Hes 32:13; 33:3-49
[l]**105:14** Mwa 35:5; 12:17-20; 20:3; Za 9:5
[m]**105:15** Mwa 26:11; 20:7; 1Sam 12:3
[n]**105:16** Isa 3:1; Law 26:26; Mwa 12:10; 41:54; 2Fal 8:1; Eze 4:16
[o]**105:17** Mwa 45:5; 37:28; Mdo 7:9
[p]**105:18** Mwa 40:15
[q]**105:19** Mwa 12:10; 41:40; 40:20-21
[r]**105:20** Mwa 41:14
[s]**105:22** Mwa 41:43-44; 41:40
[t]**105:23** Mdo 7:15; 13:17; Mwa 46:6; 47:28; Za 78:51
[u]**105:24** Kut 1:7; Kum 26:7; Mdo 7:17
[v]**105:25** Kut 4:21; 1:6-10; Mdo 7:19

26 [a]Akamtuma Mose mtumishi wake,
pamoja na Aroni, aliyemchagua.
27 [b]Walifanya ishara zake za ajabu
miongoni mwao,
miujiza yake katika nchi ya Hamu.
28 [c]Alituma giza na nchi ikajaa giza,
kwani si walikuwa wameyaasi
maneno yake?
29 [d]Aligeuza maji yao kuwa damu,
ikasababisha samaki wao kufa.
30 [e]Nchi yao ilijaa vyura tele, ambao
waliingia
hadi kwenye vyumba vya kulala
vya watawala wao.
31 [f]Alisema, yakaja makundi ya mainzi,
na viroboto katika nchi yao yote.
32 [g]Alibadilisha mvua yao ikawa mvua
ya mawe,
yenye umeme wa radi nchini yao
yote,
33 [h]akaharibu mizabibu yao na miti ya
tini,
na akaangamiza miti ya nchi yao.
34 [i]Alisema, nzige wakaja,
tunutu wasio na idadi,
35 wakala kila jani katika nchi yao,
wakala mazao ya ardhi yao.
36 [j]Kisha akawaua wazaliwa wote wa
kwanza katika nchi yao,
matunda ya kwanza ya ujana wao
wote.

37 [k]Akawatoa Israeli katika nchi
wakiwa na fedha na dhahabu
nyingi,
wala hakuna hata mmoja
kutoka kabila zao aliyejikwaa.
38 [l]Misri ilifurahi walipoondoka,
kwa sababu hofu ya Israeli ilikuwa
imewaangukia.
39 [m]Alitandaza wingu kama kifuniko,
na moto kuwamulikia usiku.
40 [n]Waliomba, naye akawaletea kware,
akawashibisha kwa mkate wa
mbinguni.
41 [o]Alipasua mwamba, maji
yakabubujika,
yakatiririka jangwani kama mto.

42 [p]Kwa maana alikumbuka ahadi yake
takatifu,
aliyompa Abrahamu mtumishi
wake.
43 [q]Aliwatoa watu wake kwa furaha,
wateule wake kwa kelele za
shangwe,
44 [r]akawapa nchi za mataifa, wakawa
warithi
wa mali wengine walikuwa
wameitaabikia:
45 [s]alifanya haya ili wayashike mausia
yake
na kuzitii sheria zake.

Msifuni BWANA.[t]

## Zaburi 106

*Wema Wa BWANA Kwa Watu Wake*

1 [u]Msifuni BWANA.

Mshukuruni BWANA, kwa kuwa ni
mwema;
upendo wake wadumu milele.

---

[a]**105:26** Kut 3:10; 4:16; Hes 33:1; 16:5; 17:5-8
[b]**105:27** Za 105:28-37; Kut 7:8; 12:51; 4:17; 10:1; 3:20; Dan 4:3
[c]**105:28** Mwa 1:4; Za 99:7; Kut 10:22; 7:22
[d]**105:29** Za 78:44; Kut 7:21
[e]**105:30** Kut 8:2, 6
[f]**105:31** Za 78:45; 107:25; 148:8; Kut 8:16-18; 8:21-24
[g]**105:32** Kut 9:22-25; Ay 38:22; Za 78:47
[h]**105:33** Za 78:47; Kut 10:5, 12
[i]**105:34** Za 107:25; Kut 10:4, 12-15; 1Fal 8:27; Yoe 1:6
[j]**105:36** Kut 4:23; 12:12
[k]**105:37** Kut 3:21, 22
[l]**105:38** Kut 15:16
[m]**105:39** Kut 13:21; 1Kor 10:1; Za 78:14; Neh 9:12
[n]**105:40** Za 78:18; Kut 16:4; Yn 6:31; Kut 16:12
[o]**105:41** Hes 20:11; 1Kor 10:4; Kut 17:6; Neh 9:15; Isa 48:21
[p]**105:42** Mwa 15:1-4, 13-16; 13:14-17
[q]**105:43** Kut 15:1-19; Za 106:12
[r]**105:44** Kum 6:10-11; Za 106:12
[s]**105:45** Kum 6:14-21; 4:1, 40; Za 105:35; 78:5-7
[t]45 Msifuni BWANA kwa Kiebrania ni Hallelu Yah.
[u]**106:1** Ezr 3:11; Za 63:7; 22:23; 103:2; 119:68; 136:1-26; Yer 33:11; Mt 19:17

2 [a]Ni nani awezaye kusimulia matendo makuu ya BWANA
au kutangaza kikamilifu sifa zake?
3 [b]Heri wale wanaodumisha haki,
ambao daima wanafanya yaliyo mema.
4 [c]Ee BWANA, unikumbuke unapowatendea mema watu wako,
uwe msaada wangu unapowaokoa,
5 [d]ili niweze kufurahia mafanikio ya wateule wako,
niweze kushiriki katika furaha ya taifa lako,
na kuungana na urithi wako katika kukusifu.

6 [e]Tumetenda dhambi, kama vile baba zetu walivyotenda,
tumekosa na tumetenda uovu.
7 [f]Wakati baba zetu walipokuwa Misri,
hawakuzingatia maajabu yako,
wala hawakukumbuka wingi wa fadhili zako,
bali waliasi kando ya bahari,
Bahari ya Shamu.
8 [g]Hata hivyo aliwaokoa kwa ajili ya jina lake,
ili apate kudhihirisha uweza wake mkuu.
9 [h]Alikemea Bahari ya Shamu, nayo ikakauka,
akawaongoza katika vilindi vyake kama vile jangwani.
10 [i]Aliwaokoa mikononi mwa adui;
kutoka mikononi mwa adui aliwakomboa.
11 [j]Maji yaliwafunika adui zao,
hakunusurika hata mmoja.
12 [k]Ndipo walipoamini ahadi zake,
nao wakaimba sifa zake.

13 [l]Lakini mara walisahau aliyowatendea,
wala hawakungojea shauri lake.
14 [m]Jangwani walitawaliwa na tamaa zao,
walimjaribu Mungu nyikani.
15 [n]Kwa hiyo aliwapa kile walichoomba,
lakini akatuma juu yao ugonjwa wa kudhoofisha.

16 [o]Kambini walimwonea wivu Mose,
na pia Aroni aliyekuwa amewekwa wakfu kwa BWANA.
17 [p]Ardhi ilifunguka ikawameza Dathani,
ikawazika Abiramu na kundi lake.
18 [q]Moto uliwaka katikati ya wafuasi wao,
mwali wa moto uliwateketeza waovu.

19 [r]Huko Horebu walitengeneza ndama,
na kuabudu sanamu ya kusubu kwa chuma.
20 [s]Waliubadilisha Utukufu wao
kwa sanamu ya fahali, ambaye hula majani.
21 [t]Walimsahau Mungu aliyewaokoa,
aliyekuwa ametenda mambo makuu huko Misri,

[a]**106:2** Za 40:5; 71:16
[b]**106:3** Yer 22:15, 16; Mt 22:37; Za 15:2; 112:5; Hos 12:6
[c]**106:4** Za 25:6-7; 77:7; Mwa 50:24
[d]**106:5** Kum 30:15; Za 1:3; 105:6; 20:5; 27:5; 47:5; 118:15; Kut 34:9
[e]**106:6** 1Fal 8:47; Neh 1:7; Dan 9:5; Rum 3:9; 2Nya 30:7; Law 26:40
[f]**106:7** Amu 3:7; Za 78:42; Kut 14:11, 12
[g]**106:8** Kut 9:16; 14:30-31; Za 80:3; 107:13; 23:3; 143:11; Isa 25:9; Yoe 2:32; Yos 7:9; Yer 14:7, 21
[h]**106:9** Nah 1:4; Isa 50:3; 63:11-14; Kut 14:21; Za 18:15; 78:13
[i]**106:10** Kut 14:30; Za 107:13; 78:42, 53; Isa 35:9; 62:12
[j]**106:11** Kut 14:28
[k]**106:12** Kut 15:1-21; Za 105:43
[l]**106:13** Kut 15:24; 16:28; Hes 27:21
[m]**106:14** 1Kor 10:9; Kut 17:2; Za 78:40; 68:7
[n]**106:15** Isa 10:16; Hes 11:33; Kut 16:13; Za 78:29
[o]**106:16** Hes 16:1-3
[p]**106:17** Kum 11:6; 15:12; Hes 16:1
[q]**106:18** Law 10:2
[r]**106:19** Kut 32:4; Mdo 7:41
[s]**106:20** Yer 2:11; Rum 1:23
[t]**106:21** Za 78:11; 75:1; Kum 10:21

22 [a]miujiza katika nchi ya Hamu
na mambo ya kutisha huko Bahari ya Shamu.
23 [b]Kwa hiyo alisema kwamba angewaangamiza:
kama Mose mteule wake,
asingesimama kati yao na Mungu
kuizuia ghadhabu yake kuwaangamiza.

24 [c]Kisha waliidharau ile nchi nzuri,
hawakuiamini ahadi yake.
25 [d]Walinung'unika ndani ya mahema yao,
wala hawakumtii BWANA.
26 [e]Kwa hiyo akaapa kwa mkono ulioinuliwa
kwamba atawafanya waanguke jangwani,
27 [f]kuwatawanya wazao wao waanguke miongoni mwa mataifa,
na kuwatawanya katika nchi zote.

28 [g]Walijifunga nira na Baali wa Peori,
wakala dhabihu zilizotolewa kwa miungu isiyo na uhai.
29 [h]Waliichochea hasira ya BWANA,
wakamkasirisha kwa matendo yao maovu,
nayo tauni ikazuka katikati yao.
30 [i]Lakini Finehasi alisimama na kuingilia kati,
nayo tauni ikazuiliwa.
31 [j]Hili likahesabiwa kwake haki,
kwa vizazi visivyo na mwisho vijavyo.
32 [k]Kwenye maji ya Meriba, walimkasirisha BWANA,
janga likampata Mose kwa sababu yao;
33 [l]kwa maana walimwasi Roho wa Mungu,
na maneno yasiyofaa yakatoka midomoni kwa Mose.

34 [m]Hawakuyaangamiza yale mataifa
kama BWANA alivyowaagiza,
35 [n]bali walijichanganya na mataifa
na wakazikubali desturi zao.
36 [o]Waliabudu sanamu zao,
zikawa mtego kwao.
37 [p]Wakawatoa wana wao
na binti zao dhabihu kwa mashetani.
38 [q]Walimwaga damu isiyo na hatia,
damu za wana wao na binti zao,
ambao waliwatoa dhabihu kwa sanamu za Kanaani,
nayo nchi ikanajisika kwa damu zao.
39 [r]Wakajinajisi wenyewe kwa yale waliyotenda;
kwa matendo yao wenyewe wakajifanyia ukahaba.

40 [s]Kwa hiyo BWANA akawakasirikia watu wake
na akauchukia sana urithi wake.
41 [t]Akawakabidhi kwa mataifa
na adui zao wakawatawala.

---

[a]**106:22** Za 78:51; Kut 3:20; Kum 4:34
[b]**106:23** Kut 32:10-14; Hes 11:2; Eze 13:5; 20:13; Kum 9:19
[c]**106:24** Ebr 3:18; Yer 3:19; Hes 14:11, 30, 31; Kum 8:7
[d]**106:25** Kut 15:24; Kum 1:27; 1Kor 10:10
[e]**106:26** Hes 14:23; Ebr 4:3; 3:17; Kum 2:14
[f]**106:27** Law 26:33
[g]**106:28** Hes 23:28; 25:2, 3; Kum 4:3; Hos 9:10; Ufu 2:14
[h]**106:29** Za 64:2; 141:4; Hes 16:46; 25:3, 8
[i]**106:30** Kut 6:25; Hes 25:8
[j]**106:31** Mwa 15:6; Za 49:11; Hes 15:11-13
[k]**106:32** Kum 1:37; Kut 17:7; Hes 20:2-13
[l]**106:33** Kut 17:4-7; 23:21; Yak 3:2; Isa 63:10; Za 107:11; 51:11; Hes 20:8-12
[m]**106:34** Amu 1:21, 27-36; 2:2; Yos 9:15; Kum 2:34; 7:2, 16; 20:10; Kut 23:24
[n]**106:35** Amu 3:5, 6; Ezr 9:1, 2
[o]**106:36** Kut 10:7; 23:33; Amu 2:12; 2Fal 17:8-11; 2Nya 33:2-7; Kum 7:10, 16
[p]**106:37** Isa 57:5; Kut 10:7; 22:20; Law 18:21; Kum 32:17; 12:31; 7:16; 1Kor 10:20; Eze 16:20-21
[q]**106:38** 2Fal 3:27; Hes 35:33; Law 18:21; Kum 18:10
[r]**106:39** Mwa 3:17; Law 18:24; Eze 20:18; Hes 15:39
[s]**106:40** Law 26:28; Kut 34:9; 9:29
[t]**106:41** Amu 2:14; Neh 9:27

42 [a]Adui zao wakawaonea
na kuwatia chini ya mamlaka yao.
43 [b]Mara nyingi aliwaokoa
lakini walikuwa wamezama
kwenye uasi,
nao wakajiharibu katika dhambi
zao.

44 [c]Lakini akaangalia mateso yao
wakati aliposikia kilio chao;
45 [d]kwa ajili yao akakumbuka agano
lake,
na kutokana na upendo wake
mkuu akapooza hasira yake.
46 [e]Akawafanya wahurumiwe
na wote waliowashikilia mateka.

47 [f]Ee Bwana Mungu wetu, tuokoe.
Tukusanye tena kutoka kwa
mataifa,
ili tuweze kulishukuru jina lako
takatifu,
na kushangilia katika sifa zako.

48 [g]Atukuzwe Bwana, Mungu wa
Israeli,
tangu milele na hata milele.
Watu wote na waseme, “Amen!”

Msifuni Bwana.

## KITABU CHA TANO

*(Zaburi 107–150)*

## Zaburi 107

*Kumsifu Mungu Kwa Wema Wake*

1 [h]Mshukuruni Bwana, kwa kuwa
yeye ni mwema,
upendo wake wadumu milele.
2 [i]Waliokombolewa wa Bwana na
waseme hivi,
wale aliowaokoa kutoka mkono
wa adui,
3 [j]wale aliowakusanya kutoka nchi
mbalimbali,
kutoka mashariki na magharibi,
kutoka kaskazini na kusini.

4 [k]Baadhi yao walitangatanga
jangwani,
hawakuona njia ya kuwafikisha
mji ambao wangeweza kuishi.
5 [l]Walikuwa na njaa na kiu,
nafsi zao zikadhoofika.
6 [m]Ndipo walipomlilia Bwana katika
shida yao,
naye akawaokoa kutoka taabu
yao.
7 [n]Akawaongoza kwa njia iliyo sawa
hadi mji ambao wangeweza
kuishi.
8 [o]Basi na wamshukuru Bwana kwa
upendo wake usiokoma,
na kwa matendo yake ya ajabu
kwa wanadamu,
9 [p]kwa maana yeye humtosheleza
mwenye kiu,
na kumshibisha mwenye njaa kwa
vitu vyema.

10 [q]Wengine walikaa gizani na katika
huzuni kuu,
wafungwa wakiteseka katika
minyororo,
11 [r]kwa sababu walikuwa wameasi
dhidi ya maneno ya Mungu

[a]**106:42** Amu 4:3
[b]**106:43** Amu 7:1-25; 2:16-19; 6:1-7; Yos 10:14; Neh 9:28
[c]**106:44** Amu 3:9; 10:10
[d]**106:45** Mwa 9:15; Lk 1:72; Za 105:8; 103:11; 17:7; Law 26:41; Mao 3:32; Kut 32:14
[e]**106:46** 1Nya 16:8; Mt 19:17; 2Nya 5:13; 7:3
[f]**106:47** Za 147:2; 105:1; 30:4; 99:3; 28:9; 107:3; Isa 11:12; 27:13; 56:8; 66:20; Yer 31:8; Lk 1:74; Eze 20:34; Mik 4:6; 2Kor 5:15
[g]**106:48** Za 41:13; 72:19
[h]**107:1** 1Nya 16:8; 2Nya 5:13; 7:3; Mt 19:17
[i]**107:2** Za 106:10; Isa 35:9
[j]**107:3** Za 106:47; Isa 49:12; Hes 1:9; Yer 29:14; Eze 39:27
[k]**107:4** Yos 5:6; Za 107:36
[l]**107:5** Kut 16:3; 15:22; 17:2
[m]**107:6** Kut 14:10; Za 50:15; Isa 41:17; Hos 5:15; Yer 29:12-14
[n]**107:7** Ezr 8:21, 36; Isa 38:12
[o]**107:8** Za 105:1; 6:4; 75:1
[p]**107:9** Za 22:26; 63:5; 23:1; 34:10; Mt 5:6; Yer 31:25; Lk 1:53; Isa 55:1; 58:11
[q]**107:10** Za 107:14; 88:6; 143:3; 102:20; Isa 9:2; 42:7, 16; 49:9; 61:1; Mik 7:9; Ay 36:8
[r]**107:11** Za 5:10; Hes 14:11; 1Fal 22:5; 2Nya 36:16

na kudharau shauri
la Aliye Juu Sana.
12 [a]Aliwatumikisha kwa kazi ngumu;
walijikwaa na hapakuwepo yeyote
wa kuwasaidia.
13 [b]Ndipo walipomlilia BWANA katika
shida yao,
naye akawaokoa kutoka taabu
yao.
14 [c]Akawatoa katika giza na huzuni
kuu
na akavunja minyororo yao.
15 [d]Basi na wamshukuru BWANA kwa
upendo wake usiokoma,
na kwa matendo yake ya ajabu
kwa wanadamu,
16 [e]kwa kuwa yeye huvunja malango ya
shaba
na kukata mapingo ya chuma.

17 [f]Wengine wakawa wapumbavu
kutokana na uasi wao,
wakapata mateso kwa sababu ya
uovu wao.
18 [g]Wakachukia kabisa vyakula vyote,
wakakaribia malango ya mauti.
19 [h]Ndipo walipomlilia BWANA katika
shida yao,
naye akawaokoa kutoka taabu
yao.
20 [i]Akalituma neno lake na kuwaponya,
akawaokoa kutoka maangamizo
yao.
21 [j]Basi na wamshukuru BWANA kwa
upendo wake usiokoma,
na kwa matendo yake ya ajabu
kwa wanadamu.
22 [k]Na watoe dhabihu za kushukuru,
na wasimulie matendo yake kwa
nyimbo za furaha.

23 [l]Wengine walisafiri baharini kwa
meli,
walikuwa wafanyabiashara
kwenye maji makuu.
24 [m]Waliziona kazi za BWANA,
matendo yake ya ajabu kilindini.
25 [n]Kwa maana alisema na kuamsha
tufani
iliyoinua mawimbi juu.
26 [o]Yakainuka juu mbinguni, yakashuka
chini hadi vilindini,
katika hatari hii ujasiri wao
uliyeyuka.
27 [p]Walipepesuka na kuyumbayumba
kama walevi,
ujanja wao ukafikia ukomo.
28 [q]Ndipo walipomlilia BWANA katika
shida yao,
naye akawatoa kwenye taabu yao.
29 [r]Akatuliza dhoruba kwa mnong'ono,
mawimbi ya bahari yakatulia.
30 [s]Walifurahi ilipokuwa shwari,
naye akawaongoza hadi bandari
waliyoitamani.
31 [t]Basi na wamshukuru BWANA kwa
upendo wake usiokoma,
na kwa matendo yake ya ajabu
kwa wanadamu.

---

[a]**107:12** Isa 63:5; Za 72:12; 2Fal 14:26
[b]**107:13** Za 106:8
[c]**107:14** Isa 9:2; 42:7; 59:9; 50:10; 60:2; 29:18; Ay 36:8; Lk 1:79; Za 86:13; 116:16; 146:7; Mdo 12:7
[d]**107:15** Za 107:8, 21, 31; 105:1; 6:4; 75:1
[e]**107:16** Isa 45:2
[f]**107:17** Za 53:1; 25:7; Law 14:1; 26:16; Isa 65:6, 7; Yer 30:14, 15; Gal 6:7, 8; Mt 1:22; Mao 3:39
[g]**107:18** Ay 3:24; 6:6; 17:16; 33:22
[h]**107:19** Za 107:13; 5:2; 34:4
[i]**107:20** Kum 32:2; Mt 8:8; 2Fal 20:4; Lk 7:7; Kut 15:26; Hes 21:8; Za 30:3; 16:10; 56:13; 147:15; Ay 33:28
[j]**107:21** Za 107:15; 6:4; 75:1
[k]**107:22** Law 7:12; Za 9:11; 73:28; 65:8; 50:14; 118:17; Ay 8:21; Ebr 13:15
[l]**107:23** Isa 42:10; Za 104:26
[m]**107:24** Za 64:9; 111:2; 143:5
[n]**107:25** Za 105:31; 50:3; 93:3
[o]**107:26** Za 22:14; Isa 13:7; Nah 2:10; Lk 8:23; Yos 2:11
[p]**107:27** Isa 19:14; 24:20; 28:7
[q]**107:28** Za 107:19; 4:1; Yon 1:6
[r]**107:29** Lk 8:24; Za 93:3; 65:7; Mk 4:39-41; Yon 1:15; Isa 50:2; Mt 8:26
[s]**107:30** Za 107:7
[t]**107:31** Za 107:15; 6:4; 75:1; 106:2

32 [a]Na wamtukuze yeye katika
kusanyiko la watu,
na wamsifu katika baraza la
wazee.

33 [b]Yeye aligeuza mito kuwa jangwa,
chemchemi za maji zitiririkazo
kuwa ardhi yenye kiu,
34 [c]nchi izaayo ikawa ya chumvi
isiyofaa,
kwa sababu ya uovu wa wale
walioishi humo.
35 [d]Aligeuza jangwa likawa madimbwi
ya maji,
nayo ardhi kame kuwa chemchemi
za maji zitiririkazo;
36 [e]aliwaleta wenye njaa wakaishi
humo,
nao wakajenga mji wangeweza
kuishi.
37 [f]Walilima mashamba na kupanda
mizabibu,
nayo ikazaa matunda mengi,
38 [g]Mungu aliwabariki, hesabu yao
ikaongezeka sana,
wala hakuruhusu mifugo yao
kupungua.

39 [h]Kisha hesabu yao ilipungua, na
walinyenyekeshwa
kwa kuonewa, maafa na huzuni.
40 [i]Yeye ambaye huwamwagia dharau
wakuu,
aliwafanya watangetange nyikani
isiyo na njia.
41 [j]Lakini yeye aliwainua wahitaji
katika taabu zao,
na kuongeza jamaa zao kama
makundi ya kondoo.
42 [k]Wanyofu wataona na kufurahi,
lakini waovu wote watafunga
vinywa vyao.

43 [l]Yeyote aliye na hekima, ayasikie
mambo haya,
na atafakari upendo mkuu wa
BWANA.

## Zaburi 108

*Kuomba Msaada Dhidi Ya Adui*

**(Zaburi 57:7-11; 60:5-12)**

*Wimbo. Zaburi ya Daudi.*

1 [m]Ee Mungu, moyo wangu ni thabiti;
nitaimba na kusifu kwa moyo
wangu wote.
2 [n]Amka, kinubi na zeze!
Nitayaamsha mapambazuko.
3 Nitakusifu wewe, Ee BWANA,
katikati ya mataifa;
nitaimba habari zako, katikati ya
jamaa za watu.
4 [o]Kwa maana upendo wako ni mkuu,
ni juu kuliko mbingu;
uaminifu wako unazifikia anga.
5 [p]Ee Mungu, utukuzwe juu ya
mbingu,
utukufu wako na uenee duniani
kote.

6 [q]Tuokoe na utusaidie kwa mkono
wako wa kuume,
ili wale uwapendao wapate
kuokolewa.

[a]**107:32** Za 30:1; 34:3; 99:5; 1:5; 22:22; 26:12; 35:18
[b]**107:33** 1Fal 17:1; Yoe 1:20; Isa 41:15; 42:15; 50:2; 34:9, 10; Eze 30:12; Nah 1:4; Za 74:15; 104:10
[c]**107:34** Mwa 13:10
[d]**107:35** 2Fal 3:17; Za 105:41; 126:4; Isa 43:19; 51:3; 35:7; Ay 38:26
[e]**107:36** Mdo 17:26
[f]**107:37** 2Fal 19:29; Isa 37:30
[g]**107:38** Mwa 12:2; 49:25; Kum 7:13
[h]**107:39** 2Fal 10:32; Eze 5:12; Za 44:9
[i]**107:40** Ay 12:18, 21; Kum 32:10
[j]**107:41** 1Sam 2:8; 2Sam 7:8; Za 113:7-9; Ay 21:11; 8:7
[k]**107:42** Ay 22:19; 5:16; Mit 10:11; Rum 3:19; Za 97:10-12
[l]**107:43** Yer 9:12; Hos 14:9; Za 103:11; Dan 12:10
[m]**108:1** Za 112:7; 119:30, 112; 18:49
[n]**108:2** Ay 21:12
[o]**108:4** Hes 14:18; Kum 7:9; Kut 34:6; Za 36:5; Mik 7:18-20
[p]**108:5** Za 8:1; 57:5
[q]**108:6** Ay 40:14

7 [a]Mungu amenena kutoka patakatifu
pake:
"Nitaigawa Shekemu kwa ushindi
na kulipima Bonde la Sukothi.
8 [b]Gileadi ni yangu, Manase ni yangu,
Efraimu ni kofia yangu ya chuma,
nayo Yuda ni fimbo yangu ya
utawala.
9 [c]Moabu ni sinia langu la kunawia,
juu ya Edomu natupa kiatu
changu;
nashangilia kwa kushindwa kwa
Ufilisti."

10 [d]Ni nani atakayenipeleka hadi mji
wenye ngome?
Ni nani atakayeniongoza hadi
nifike Edomu?
11 [e]Ee Mungu, si ni wewe uliyetukataa
sisi,
na hutoki tena na majeshi yetu?
12 [f]Tuletee msaada dhidi ya adui,
kwa maana msaada wa
mwanadamu haufai kitu.
13 [g]Kwa msaada wa Mungu tutapata
ushindi,
naye atawaponda adui zetu.

## Zaburi 109

*Lalamiko La Mtu Aliyeko Kwenye Shida*

*Kwa mwimbishaji. Zaburi ya Daudi.*

1 [h]Ee Mungu, ambaye ninakusifu,
usiwe kimya,
2 [i]kwa maana watu waovu na
wadanganyifu
wamefungua vinywa vyao dhidi
yangu;
wasema dhidi yangu
kwa ndimi za udanganyifu.
3 [j]Wamenizunguka kwa maneno ya
chuki,
wananishambulia bila sababu.
4 [k]Wanachonilipa badala ya urafiki
wangu ni kunishtaki,
lakini mimi ninawaombea.
5 [l]Wananilipiza mabaya kwa mema,
chuki badala ya urafiki wangu.

6 [m]Agiza mtu mwovu ampinge,
mshtaki[n] asimame mkono wake wa
kuume.
7 [o]Anapohukumiwa, apatikane na
hatia,
nayo maombi yake yamhukumu.
8 [p]Siku zake za kuishi na ziwe chache,
nafasi yake ya uongozi ichukuliwe
na mtu mwingine.
9 [q]Watoto wake na waachwe yatima,
mke wake na awe mjane.
10 [r]Watoto wake na watangetange
wakiomba,
na wafukuzwe kwenye magofu ya
nyumba zao.
11 [s]Mtu anayemdai na ateke vyote
alivyo navyo,
matunda ya kazi yake yatekwe
nyara na wageni.
12 [t]Asiwepo mtu yeyote wa kumtendea
mema
wala wa kuwahurumia yatima
wake.
13 [u]Uzao wake na ukatiliwe mbali,
majina yao yafutike katika kizazi
kifuatacho.

---

[a]**108:7** Za 89:35; 68:35; 102:19; Mwa 12:6; 33:17
[b]**108:8** Za 78:68; Mwa 49:10
[c]**108:9** Mwa 19:37; 2Sam 8:1, 13-14
[d]**108:10** Za 60:9
[e]**108:11** Za 44:9
[f]**108:12** Isa 10:3; 30:3, 5; 31:3; Yer 2:36; 17:7; Za 118:8; 146:3
[g]**108:13** Za 44:5; Isa 22:5; 63:3, 6; 25:10; Mao 1:15; Mal 4:3; Ufu 14:9
[h]**109:1** Kut 15:2; Yer 17:14; Ay 34:29; Za 83:1
[i]**109:2** Za 43:1; 52:4
[j]**109:3** Za 69:4; 35:7; 35:7, 10; Yn 15:25; 1Sam 19:4, 5
[k]**109:4** Za 69:13; 141:5
[l]**109:5** Mwa 44:4; Za 38:20
[m]**109:6** 1Nya 21:1; Ay 1:6; Zek 3:1
[n]6 Mshtaki hapa maana yake ni Shetani.
[o]**109:7** Za 1:5; Mit 28:9; Zek 3:1
[p]**109:8** Ay 15:32; Mdo 1:20
[q]**109:9** Kut 22:24; Yer 18:21
[r]**109:10** Mwa 4:12
[s]**109:11** Hes 14:3; Isa 1:7; 6:11; 36:1; Mao 5:2; Neh 5:3; Ay 20:18; 18:9
[t]**109:12** Ay 5:4
[u]**109:13** Za 21:10; 9:5; 37:28; Hes 14:12; Mit 10:7; Ay 18:19

14 [a]Maovu ya baba zake na
yakumbukwe
mbele za BWANA,
dhambi ya mama yake
isifutwe kamwe.
15 [b]Dhambi zao na zibaki daima mbele
za BWANA,
ili apate kukatilia mbali
kumbukumbu lao duniani.

16 [c]Kwa maana kamwe hakuweza
kutenda wema,
bali alimfukuza mnyonge na
mhitaji,
aliwafanyia jeuri wahitaji na
waliovunjika moyo.
17 [d]Alipenda kulaani,
nayo laana ikampata;
hakupenda kubariki,
kwa hiyo baraka na ikae mbali
naye.
18 [e]Alivaa kulaani kama vazi lake,
nayo laana ikamwingia mwilini
mwake kama maji,
kwenye mifupa yake kama mafuta.
19 [f]Na iwe kama joho alilozungushiwa,
kama mshipi aliofungiwa daima.
20 [g]Haya na yawe malipo ya BWANA
kwa washtaki wangu,
kwa wale wanaoninenea mabaya.

21 [h]Lakini wewe, Ee BWANA Mwenyezi,
unitendee wema kwa ajili ya jina
lako,
uniokoe kwa wema wa pendo
lako.
22 Maana mimi ni maskini na mhitaji,
moyo wangu umejeruhiwa ndani
yangu.
23 [i]Ninafifia kama kivuli cha jioni,
nimerushwa-rushwa kama nzige.
24 [j]Magoti yangu yamelegea kwa
kufunga,
mwili wangu umedhoofika na
kukonda.
25 [k]Nimekuwa kitu cha kudharauliwa
kwa washtaki wangu,
wanionapo, hutikisa vichwa vyao.

26 [l]Ee BWANA, Mungu wangu nisaidie,
niokoe sawasawa na upendo
wako.
27 [m]Watu na wafahamu kuwa ni mkono
wako,
kwamba wewe, Ee BWANA,
umetenda hili.
28 [n]Wanaweza kulaani, lakini wewe
utabariki,
watakaposhambulia wataaibishwa,
lakini mtumishi wako atashangilia.
29 [o]Washtaki wangu watavikwa
fedheha,
na kufunikwa na aibu kama joho.

30 [p]Kwa kinywa changu nitamtukuza
sana BWANA,
katika umati mkubwa nitamsifu.
31 [q]Kwa maana husimama mkono wa
kuume wa mhitaji,
kuokoa maisha yake kutoka kwa
wale wanaomhukumu.

## Zaburi 110

*BWANA Na Mfalme Wake Mteule*

*Zaburi ya Daudi.*

1 [r]BWANA amwambia Bwana wangu:
"Keti mkono wangu wa kuume,

[a]**109:14** Kut 20:5
[b]**109:15** Za 90:8; Kut 17:14; Kum 32:26; Ay 18:17
[c]**109:16** Ay 20:19; Za 35:10; 34:18
[d]**109:17** Mit 28:27; Mt 7:2
[e]**109:18** Za 10:7; Hes 5:22
[f]**109:19** Za 109:29; 73:6; Eze 7:27
[g]**109:20** Kut 32:34; Za 54:5; 94:23; 7:10; Isa 3:11; 2Tim 4:14
[h]**109:21** Kut 9:16; Za 3:7; 23:3; 69:16
[i]**109:23** Ay 14:2
[j]**109:24** Ebr 12:12; Ay 16:8; Za 35:13
[k]**109:25** Za 22:6; Ay 16:4; Mt 27:39; Mk 15:29; Isa 37:22
[l]**109:26** Za 12:1; 119:86
[m]**109:27** Ay 37:7
[n]**109:28** 2Sam 16:12; Za 66:4; Isa 35:10; 51:11; 54:1; 65:14; Hes 22:12
[o]**109:29** Za 35:26
[p]**109:30** Za 35:18
[q]**109:31** Za 16:8; 108:6
[r]**110:1** Mt 22:44; Lk 20:42; Mdo 2:34; Mk 12:36; 16:19; Ebr 1:13; 12:2; Yos 10:24; 1Fal 5:3; 1Kor 15:25; Za 45:6

mpaka nitakapowafanya adui zako
kuwa mahali pa kuweka miguu
yako."

2 [a]BWANA ataeneza fimbo yako ya
utawala yenye nguvu kutoka
Sayuni;
utatawala katikati ya adui zako.
3 [b]Askari wako watajitolea kwa hiari
katika siku yako ya vita.
Ukiwa umevikwa fahari takatifu,
kutoka tumbo la mapambazuko
utapokea umande wa ujana wako.[c]

4 [d]BWANA ameapa,
naye hatabadilisha mawazo yake:
"Wewe ni kuhani milele,
kwa mfano wa Melkizedeki."

5 [e]Bwana yuko mkono wako wa
kuume,
atawaponda wafalme siku ya
ghadhabu yake.
6 [f]Atawahukumu mataifa, akilundika
mizoga
na kuwaponda watawala wa dunia
nzima.
7 [g]Atakunywa maji katika kijito kando
ya njia,[h]
kwa hiyo atainua kichwa chake
juu.

## Zaburi 111[i]

*Sifa Za BWANA Kwa Matendo Ya Ajabu*

1 [j]Msifuni BWANA.

Nitamtukuza BWANA kwa moyo
wangu wote,
katika baraza la wanyofu na katika
kusanyiko.

2 [k]Kazi za BWANA ni kuu,
wote wanaopendezwa nazo
huzitafakari.
3 [l]Kazi zake zimejaa fahari na utukufu,
haki yake hudumu daima.
4 [m]Amefanya maajabu yake
yakumbukwe,
BWANA ni mwenye neema na
huruma.
5 [n]Huwapa chakula wale wanaomcha,
hulikumbuka agano lake milele.
6 [o]Amewaonyesha watu wake uwezo
wa kazi zake,
akiwapa nchi za mataifa mengine.
7 [p]Kazi za mikono yake ni za uaminifu
na haki,
mausia yake yote ni ya kuaminika.
8 [q]Zinadumu milele na milele,
zikifanyika kwa uaminifu na
unyofu.
9 [r]Aliwapa watu wake ukombozi,
aliamuru agano lake milele:
jina lake ni takatifu na la
kuogopwa.

10 [s]Kumcha BWANA ndicho chanzo cha
hekima,
wote wanaozifuata amri zake
wana busara.
Sifa zake zadumu milele.

[a]**110:2** Mwa 49:10; Za 45:6; 2:6; 72:8; Isa 14:5; Yer 48:17
[b]**110:3** Kut 15:11; Mik 5:7
[c]3 Au: vijana wako watakujia kama umande.
[d]**110:4** Hes 23:19; Zek 6:13; Ebr 5:6; 5:10; 7:15-17; 7:21; Mwa 14:18
[e]**110:5** Za 16:8; 2:12; 68:21; 76:12; Kum 7:24; Isa 60:12; Dan 2:44; Za 2:5; Rum 2:5; Ufu 6:17; 11:18
[f]**110:6** Za 9:19; 18:38; Isa 5:25; 34:3; 66:24
[g]**110:7** Za 3:3; 27:6
[h]7 Au: Yeye atoaye mtu wa kurithi mwingine atamweka kwenye mamlaka.
[i]Zaburi hii imetungwa kila mstari ukianzia na herufi ya alfabeti ya Kiebrania zikifuatana tangu Aleph (A) hadi Taw (T); zote ni 22.
[j]**111:1** Za 34:1; 109:30; 115:18; 145:10; 9:1; 89:7; 1:5
[k]**111:2** Ay 36:24; Za 143:5; 64:9; Ufu 15:3
[l]**111:3** Za 112:3, 9; 119:142
[m]**111:4** Kum 4:31; Za 86:15
[n]**111:5** Mwa 1:30; Za 37:25; 103:11; 105:8; Mt 6:26, 31-33; 1Nya 16:15
[o]**111:6** Za 64:9; 66:3; 105:44
[p]**111:7** Za 92:4; 19:7; 119:128
[q]**111:8** Za 119:89, 152, 160; Isa 40:8; Mt 5:18
[r]**111:9** Za 34:22; 103:4; 130:7; 30:4; 99:3; Lk 1:68; 1:49
[s]**111:10** Ay 23:15; Kum 4:6; Za 19:9; 119:98, 104, 130; 28:6; 89:52

## Zaburi 112[a]

*Baraka Za Mwenye Haki*

1 [b]Msifuni BWANA.

Heri mtu yule amchaye BWANA,
mtu yule apendezwaye sana na
amri zake.

2 [c]Watoto wake watakuwa wenye
uwezo katika nchi,
kizazi cha watu waadilifu
kitabarikiwa.
3 [d]Nyumbani mwake kuna mali na
utajiri,
haki yake hudumu milele.
4 [e]Hata gizani nuru humzukia mtu
mwadilifu,
yule mwenye rehema, huruma na
haki.

5 [f]Mema yatamjia mtu yule aliye
mkarimu na mwenye
kukopesha bila riba,
anayefanya mambo yake kwa
haki.
6 [g]Hakika hatatikisika kamwe,
mtu mwenye haki atakumbukwa
milele.
7 [h]Hataogopa habari mbaya,
moyo wake ni thabiti,
ukimtegemea BWANA.
8 [i]Moyo wake ni salama, hatakuwa na
hofu,
mwishoni ataona ushindi dhidi ya
adui zake.
9 [j]Ametawanya vipawa vyake kwa
ukarimu akawapa maskini;
haki yake hudumu milele;
pembe yake itatukuzwa kwa
heshima.

10 [k]Mtu mwovu ataona na kuchukizwa,
atasaga meno yake na kutoweka,
kutamani kwa mtu mwovu
kutaishia patupu.

## Zaburi 113

*Kumsifu BWANA Kwa Wema Wake*

1 [l]Msifuni BWANA.

Enyi watumishi wa BWANA msifuni,
lisifuni jina la BWANA.
2 [m]Jina la BWANA na lisifiwe,
sasa na hata milele.
3 [n]Kuanzia mawio ya jua hadi
machweo yake,
jina la BWANA linapaswa kusifiwa.

4 [o]BWANA ametukuka juu ya mataifa
yote,
utukufu wake juu ya mbingu.
5 [p]Ni nani aliye kama BWANA Mungu
wetu,
Yeye ambaye ameketi juu kwenye
kiti cha enzi,
6 [q]ambaye huinama atazame chini
aone mbingu na nchi?

7 [r]Huwainua maskini kutoka
mavumbini,
na kuwanyanyua wahitaji kutoka
kwenye jalala,
8 [s]huwaketisha pamoja na wakuu,
pamoja na wakuu wa watu wake.

---

[a]Zaburi hii imetungwa kila mstari ukianzia na herufi ya alfabeti ya Kiebrania zikifuatana tangu Aleph (A) hadi Taw (T); zote ni 22.
[b]**112:1** Za 33:2; 103:1; 150:1; 1:1, 2; Ay 1:8; Za 103:11; 115:13; 128:1; 1:2; 119:14, 16, 47, 92
[c]**112:2** Za 25:13; 37:26; 128:2-4
[d]**112:3** Kum 8:18; Za 37:6; 111:3
[e]**112:4** Za 18:28; 5:12
[f]**112:5** Za 37:21, 26; Lk 6:35
[g]**112:6** Za 15:5; 55:22; Mit 10:7; Mhu 2:16
[h]**112:7** Za 57:7; 108:1; 28:7; 56:3-4; Isa 12:2
[i]**112:8** Za 3:6; 27:1; 54:7; 56:11; Mit 1:33; Isa 12:2
[j]**112:9** Lk 19:8; Mdo 9:36; 2Kor 9:9; Za 111:3; 75:10
[k]**112:10** Za 86:17; 34:21; 37:12; Mt 8:12; Ay 8:13
[l]**113:1** Za 22:23; 34:22; 103:21; 134:1
[m]**113:2** Za 30:4; 48:10; 145:21; 148:13; 149:3; 115:18; 131:3; Isa 12:4; Dan 2:20
[n]**113:3** Isa 24:15; 45:6; 59:19; Mal 1:11
[o]**113:4** Za 99:2; 8:1; 57:11
[p]**113:5** Kut 8:10; Ay 16:19; Za 35:10; 103:19
[q]**113:6** Za 11:4; 138:6; Isa 57:15
[r]**113:7** 1Sam 2:8; Za 35:10; 68:10; 140:12; 107:41
[s]**113:8** 2Sam 9:11

9 [a]Humjalia mwanamke tasa kutulia
nyumbani mwake,
akiwa mama watoto mwenye
furaha.

Msifuni BWANA.

## Zaburi 114

*Maajabu Ya Mungu Wakati Israeli Walipotoka Misri*

1 [b]Wakati Israeli walipotoka Misri,
nyumba ya Yakobo kutoka kwa
watu wa lugha ngeni,
2 [c]Yuda alifanywa makao matakatifu
ya Mungu,
Israeli akawa milki yake.

3 [d]Bahari ilitazama ikakimbia,
Yordani ulirudi nyuma,
4 [e]milima ilirukaruka kama kondoo
dume,
vilima kama wana-kondoo.

5 [f]Ee bahari, ni nini kilichokufanya
ukakimbia,
nawe, ee Yordani, ukarudi nyuma,
6 enyi milima mkarukaruka kama
kondoo dume,
enyi vilima, kama wana-kondoo?

7 [g]Ee dunia, tetemeka mbele za Bwana,
mbele za Mungu wa Yakobo,
8 [h]aliyegeuza mwamba kuwa dimbwi
la maji,
mwamba mgumu kuwa
chemchemi za maji.

## Zaburi 115

*Mungu Mmoja Wa Kweli*

1 [i]Sio kwetu sisi, Ee BWANA, sio kwetu
sisi,
bali utukufu ni kwa jina lako,
kwa sababu ya upendo
na uaminifu wako.

2 [j]Kwa nini mataifa waseme,
"Yuko wapi Mungu wao?"
3 [k]Mungu wetu yuko mbinguni,
naye hufanya lolote limpendezalo.
4 [l]Lakini sanamu zao ni za fedha na
dhahabu,
zilizotengenezwa kwa mikono ya
wanadamu.
5 [m]Zina vinywa, lakini haziwezi
kusema,
zina macho, lakini haziwezi
kuona;
6 zina masikio, lakini haziwezi kusikia,
zina pua, lakini haziwezi kunusa;
7 zina mikono, lakini haziwezi
kupapasa,
zina miguu, lakini haziwezi
kutembea;
wala koo zao haziwezi kutoa sauti.
8 [n]Wale wanaozitengeneza watafanana
nazo,
vivyo hivyo wale wote
wanaozitumainia.

9 [o]Ee nyumba ya Israeli, mtumainini
BWANA,
yeye ni msaada na ngao yao.
10 [p]Ee nyumba ya Aroni, mtumainini
BWANA,
yeye ni msaada na ngao yao.
11 [q]Ninyi mnaomcha, mtumainini
BWANA,
yeye ni msaada na ngao yao.

---

[a]**113:9** 1Sam 2:5
[b]**114:1** Kut 13:3; 29:46
[c]**114:2** Kut 15:17; Za 76:1; 78:68, 69
[d]**114:3** Kut 14:21; Za 77:16; Kut 15:8; Yos 3; 16
[e]**114:4** Amu 5:5
[f]**114:5** Kut 14:21
[g]**114:7** Kut 15:14; 1Nya 16:30
[h]**114:8** Kut 17:6; Hes 20:11
[i]**115:1** Za 29:2; 96:8; Kut 34:6
[j]**115:2** Za 42:3, 10; 79:10; Yoe 2:17
[k]**115:3** Ezr 5:11; Neh 1:4; Za 136:26; 135:6; 103:19; Mit 6:9; Dan 4:35; 1Nya 16:26
[l]**115:4** 2Fal 19:18; 2Nya 32:19; Yer 10:3-5; Mdo 19:26; Kum 4:28; Ufu 9:20; Za 135:15, 16; Isa 40:19; Hos 8:6; 1Kor 10:19, 20
[m]**115:5** Yer 10:5
[n]**115:8** Za 135:18; Isa 44:9, 10; Yon 2:8; Hab 2:18
[o]**115:9** Za 37:3; 62:8; 33:20; Mit 30:5
[p]**115:10** Kut 30:30; Za 118:3; Mal 2:7
[q]**115:11** Za 22:23; 103:11; 118:4

12 [a]BWANA anatukumbuka na
atatubariki:
ataibariki nyumba ya Israeli,
ataibariki nyumba ya Aroni,
13 [b]atawabariki wale wanaomcha
BWANA,
wadogo kwa wakubwa.

14 [c]BWANA na awawezeshe kuongezeka,
ninyi na watoto wenu.
15 [d]Mbarikiwe na BWANA
Muumba wa mbingu na dunia.

16 [e]Mbingu zilizo juu sana ni mali ya
BWANA,
lakini dunia amempa
mwanadamu.
17 [f]Sio wafu wanaomsifu BWANA,
wale washukao mahali pa kimya,[g]
18 [h]bali ni sisi tunaomtukuza BWANA,
sasa na hata milele.

Msifuni BWANA.[i]

### Zaburi 116

*Shukrani Kwa Kuokolewa Kutoka Mauti*

1 [j]Ninampenda BWANA kwa maana
amesikia sauti yangu;
amesikia kilio changu ili
anihurumie.
2 [k]Kwa sababu amenitegea sikio lake,
nitamwita siku zote za maisha
yangu.
3 [l]Kamba za mauti zilinizunguka,
maumivu makuu ya kuzimu
yalinipata,
nikalemewa na taabu na huzuni.
4 [m]Ndipo nikaliitia jina la BWANA:
"Ee BWANA, niokoe!"

5 [n]BWANA ni mwenye neema na haki,
Mungu wetu ni mwingi wa
huruma.
6 [o]BWANA huwalinda wanyenyekevu,
nilipokuwa katika shida kubwa,
aliniokoa.

7 [p]Ee nafsi yangu, tulia tena,
kwa kuwa BWANA amekuwa
mwema kwako.
8 [q]Kwa kuwa wewe, Ee BWANA,
umeniokoa nafsi yangu na mauti,
macho yangu kutokana na machozi,
miguu yangu kutokana na
kujikwaa,
9 [r]ili niweze kutembea mbele za
BWANA,
katika nchi ya walio hai.
10 [s]Niliamini, kwa hiyo nilisema,
"Mimi nimeteseka sana."
11 [t]Katika taabu yangu nilisema,
"Wanadamu wote ni waongo."

12 [u]Nimrudishie BWANA nini
kwa wema wake wote
alionitendea?
13 [v]Nitakiinua kikombe cha wokovu
na kulitangaza jina la BWANA.

---

[a]**115:12** 1Nya 16:15; Mwa 12:2; Efe 1:3
[b]**115:13** Za 24:4; 112:1; Law 26:3; Mit 10:6; Kum 11:27
[c]**115:14** Kum 1:11
[d]**115:15** Mdo 14:15; Ufu 10:6; Za 96:5; Mwa 1:1; 14:19
[e]**115:16** Za 89:11; Mwa 1:28; 8:6-8
[f]**115:17** Za 88:10-12
[g]17 Mahali pa kimya maana yake ni Kuzimu, yaani Sheol kwa Kiebrania.
[h]**115:18** Za 111:1; 113:2; 28:6; 33:2; 105:1; 145:2; Dan 2:20
[i]18 Msifuni BWANA ni Kiebrania Hallelu Yah.
[j]**116:1** Za 18:1; 31:22; 40:1; 6:9; 28:2
[k]**116:2** Za 5:1
[l]**116:3** 2Sam 22:6; Za 18:4-5
[m]**116:4** Za 80:2, 18; 118:5
[n]**116:5** Kut 22:27; 9:27; Ezr 9:15; Za 11:7; 86:15; 2Nya 12:6; Neh 9:8; Yer 12:1; Mao 1:18; Ufu 16:5
[o]**116:6** Za 79:8; 18:3; 22:5; 107:13
[p]**116:7** Za 13:6; 106:1; 142:7; 46:10; 62:1; 131:2; Mt 11:29; Yer 6:16
[q]**116:8** Za 86:13
[r]**116:9** Mwa 5:22; Za 56:13; 89:15; 27:13; Ay 28:13; Isa 38:11; Yer 11:9
[s]**116:10** Za 9:18; 72:2; 107:17; 119:67, 71, 75; 2Kor 4:13
[t]**116:11** Yer 9:3-5
[u]**116:12** Za 103:2; 106:1
[v]**116:13** Za 105:1

14 [a]Nitazitimiza nadhiri zangu kwa
BWANA
mbele za watu wake wote.

15 [b]Kifo cha watakatifu kina thamani
machoni pa BWANA.
16 [c]Ee BWANA, hakika mimi ni
mtumishi wako,
mimi ni mtumishi wako,
mwana wa mjakazi wako;[d]
umeniweka huru
toka katika minyororo yangu.

17 [e]Nitakutolea dhabihu ya
kukushukuru
na kuliita jina la BWANA.
18 [f]Nitazitimiza nadhiri zangu kwa
BWANA
mbele za watu wake wote,
19 [g]katika nyua za nyumba ya BWANA,
katikati yako, ee Yerusalemu.

Msifuni BWANA.

### Zaburi 117

*Sifa Za BWANA*

1 [h]Msifuni BWANA, enyi mataifa yote;
mtukuzeni yeye, enyi watu wote.
2 [i]Kwa kuwa upendo wake kwetu ni
mkuu,
uaminifu wa BWANA unadumu
milele.

Msifuni BWANA.

### Zaburi 118

*Shukrani Kwa Ajili Ya Ushindi*

1 [j]Mshukuruni BWANA, kwa kuwa ni
mwema;
upendo wake wadumu milele.
2 [k]Israeli na aseme sasa:
"Upendo wake wadumu milele."
3 [l]Nyumba ya Aroni na iseme sasa:
"Upendo wake wadumu milele."
4 [m]Wote wamchao BWANA na waseme
sasa:
"Upendo wake wadumu milele."

5 [n]Wakati wa maumivu yangu makuu
nilimlilia BWANA,
naye akanijibu kwa kuniweka
huru.
6 [o]BWANA yuko pamoja nami,
sitaogopa.
Mwanadamu anaweza kunitenda
nini?
7 [p]BWANA yuko pamoja nami,
yeye ni msaidizi wangu.
Nitawatazama adui zangu
wakiwa wameshindwa.

8 [q]Ni bora kumkimbilia BWANA
kuliko kumtumainia mwanadamu.
9 [r]Ni bora kumkimbilia BWANA
kuliko kuwatumainia wakuu.

10 [s]Mataifa yote yalinizunguka,
lakini kwa jina la BWANA
naliwakatilia mbali.
11 [t]Walinizunguka pande zote,
lakini kwa jina la BWANA
naliwakatilia mbali.
12 [u]Walinizunguka kama kundi la
nyuki,
lakini walikufa haraka kama miiba
iteketeayo;
kwa jina la BWANA naliwakatilia
mbali.

---

[a] **116:14** Hes 30:2; Za 66:13
[b] **116:15** Za 72:14; Hes 23:10; Ay 5:26; Lk 16:22; Ufu 14:13
[c] **116:16** Za 119:125; 143:12; 86:16; Ay 12:18
[d] 16 Au: mwanao mwaminifu.
[e] **116:17** Law 7:12; Ezr 1:4
[f] **116:18** Za 116:14; Law 22:18
[g] **116:19** Za 102:21; 92:13; 135:2; 96:8; 100:4
[h] **117:1** Za 22:23; 103:2; Rum 15:11
[i] **117:2** Za 17:7; 103:11; 119:90; 146:6
[j] **118:1** 1Nya 16:8; Ezr 3:11; 2Nya 7:3; 5:13
[k] **118:2** Za 115:9; 106:1; 136:1-26
[l] **118:3** Kut 30:30; Za 115:10
[m] **118:4** Za 115:11
[n] **118:5** Za 18:6; 31:7; 77:2; 120:1; 118:21; 34:4; 86:7; 116:1; 138:3
[o] **118:6** Kum 31:6; Ebr 13:5; Za 56:5
[p] **118:7** Kum 33:29; Ebr 13:6; Za 54:4
[q] **118:8** Yer 17:5, 7; Za 9:9; 62:8; 5:11; 37:3; 40:4; 108:12; Isa 25:4; 57:13; 2:22; 2Nya 32:7-8
[r] **118:9** Za 146:3; Isa 30:2, 3
[s] **118:10** Za 37:9
[t] **118:11** Za 88:17; 3:6
[u] **118:12** Mhu 7:6; Za 58:9; 37:9; Kum 1:44

13 [a]Nilisukumwa nyuma karibu
kuanguka,
lakini BWANA alinisaidia.
14 [b]BWANA ni nguvu yangu na wimbo
wangu,
yeye amefanyika wokovu wangu.

15 [c]Sauti za shangwe na ushindi
zinavuma hemani mwa wenye
haki:
"Mkono wa kuume wa BWANA
umetenda mambo makuu!
16 [d]Mkono wa kuume wa BWANA
umeinuliwa juu,
mkono wa kuume wa BWANA
umetenda mambo makuu!"

17 [e]Sitakufa, bali nitaishi,
nami nitatangaza yale BWANA
aliyoyatenda.
18 [f]BWANA ameniadhibu vikali,
lakini hakuniacha nife.

19 [g]Nifungulie malango ya haki,
nami nitaingia na kumshukuru
BWANA.
20 [h]Hili ni lango la BWANA
ambalo wenye haki wanaweza
kuliingia.
21 [i]Nitakushukuru, kwa kuwa ulinijibu,
umekuwa wokovu wangu.

22 [j]Jiwe walilolikataa waashi,
limekuwa jiwe kuu la pembeni.
23 [k]BWANA ametenda hili,
nalo ni la kushangaza machoni
petu.
24 [l]Hii ndiyo siku BWANA aliyoifanya,
tushangilie na kufurahi ndani
yake.

25 [m]Ee BWANA, tuokoe,
Ee BWANA, utujalie mafanikio.
26 [n]Heri yule ajaye kwa jina la BWANA.
Kutoka nyumba ya BWANA
tunakubariki.
27 [o]BWANA ndiye Mungu,
naye ametuangazia nuru yake.
Mkiwa na matawi mkononi,
unganeni kwenye maandamano ya
sikukuu
hadi kwenye pembe za
madhabahu.

28 [p]Wewe ni Mungu wangu,
nitakushukuru,
wewe ni Mungu wangu,
nitakutukuza.

29 Mshukuruni BWANA kwa kuwa ni
mwema;
upendo wake wadumu milele.

## Zaburi 119[q]

*Sifa Za Sheria Ya BWANA*

*Kujifunza Sheria Ya BWANA*

1 [r]Heri wale walio waadilifu katika
njia zao,
wanaoenenda katika sheria ya
BWANA.

---

[a]**118:13** Za 118:7; 86:17; 2Nya 18:31
[b]**118:14** Kut 15:2; Za 62:2
[c]**118:15** Ay 8:21; Lk 1:51; Za 106:5; 89:13; 108:6; Kut 15:6
[d]**118:16** Kut 15:6
[e]**118:17** Hab 1:12; Za 6:5; 64:9; 71:16; 73:28; Kum 32:3
[f]**118:18** Yer 31:18; Ebr 12:5; 1Kor 11:32; Za 86:13; Mit 3:11, 12
[g]**118:19** Isa 26:2; Za 24:7; 100:4
[h]**118:20** Ufu 22:14; Za 122:1, 2; 15:1, 2; 24:3-4
[i]**118:21** Za 118:5; 27:1
[j]**118:22** Mdo 4:11; Isa 8:14; 17:10; 19:13; 28:16; Mt 21:42; Lk 20:17; Zek 4:7; 10:4; Mk 12:10; 1Pet 2:7; Efe 2:20
[k]**118:23** Ay 5:9; Mt 21:42; Mk 12:11
[l]**118:24** Za 70:4; 2Kor 6:2
[m]**118:25** Za 28:9; 116:4
[n]**118:26** Zek 4:7; Mt 11:3; 21:9; 23:39; Mk 11:9; Lk 13:35; 19:38; Yn 12:13; Za 129:8
[o]**118:27** Za 27:1; Mal 4:2; Isa 60:1; 58:10; 19:20; 1Fal 18:21; 1Pet 2:9; Mik 7:9; Law 23:40; Es 8:2; Kut 27:2
[p]**118:28** Mwa 28:21; Za 16:2; 63:1; Isa 25:1; Kut 15:2
[q]Zaburi hii imetungwa kila beti likianzia, na pia kila mstari katika lile beti, na herufi 22 za alfabeti ya Kiebrania zikifuatana tangu Aleph (A) hadi Taw (T).
[r]**119:1** Mwa 17:1; Za 1:2; 128:1; Kum 18:13; Mit 11:20

[2] [a]Heri wale wanaozishika shuhuda zake,
wamtafutao kwa moyo wao wote.
[3] [b]Wasiofanya lolote lililo baya,
wanaoenenda katika njia zake.
[4] [c]Umetoa maagizo yako
ili tuyatii kwa ukamilifu.
[5] [d]Laiti mwenendo wangu ungekuwa imara
katika kuyatii maagizo yako!
[6] [e]Hivyo mimi sitaaibishwa
ninapozingatia amri zako zote.
[7] [fg]Nitakusifu kwa moyo mnyofu
ninapojifunza sheria zako za haki.
[8] [h]Nitayatii maagizo yako;
usiniache kabisa.

*Kutii Sheria Ya Bwana*

[9] [i]Kijana aifanye njia yake kuwa safi jinsi gani?
Ni kwa kutii, akilifuata neno lako.
[10] [j]Ninakutafuta kwa moyo wangu wote,
usiniache niende mbali na amri zako.
[11] [k]Nimelificha neno lako moyoni mwangu
ili nisikutende dhambi.
[12] [l]Sifa ni zako, Ee Bwana,
nifundishe maagizo yako.
[13] [m]Kwa midomo yangu nitasimulia sheria zote
zinazotoka katika kinywa chako.
[14] [n]Ninafurahia kufuata sheria zako
kama mtu afurahiaye mali nyingi.
[15] [o]Ninatafakari maagizo yako
na kuziangalia njia zako.
[16] [p]Ninafurahia maagizo yako,
wala sitalipuuza neno lako.

*Furaha Katika Sheria Ya Bwana*

[17] [q]Mtendee mema mtumishi wako, nami nitaishi;
nitalitii neno lako.
[18] Yafungue macho yangu nipate kuona
mambo ya ajabu katika sheria yako.
[19] [r]Mimi ni mgeni duniani,
usinifiche amri zako.
[20] [s]Nafsi yangu inataabika kwa shauku kubwa
juu ya sheria zako wakati wote.
[21] [t]Unawakemea wenye majivuno, waliolaaniwa
waendao mbali na amri zako.
[22] [u]Niondolee dharau na dhihaka,
kwa kuwa ninazishika sheria zako.
[23] Ingawa watawala huketi pamoja na kunisingizia,
mtumishi wako atatafakari juu ya maagizo yako.
[24] Sheria zako ni furaha yangu,
nazo ni washauri wangu.

*Kuamua Kuitii Sheria Ya Bwana*

[25] [v]Nimelazwa chini mavumbini,
yahifadhi maisha yangu sawasawa na neno lako.
[26] [w]Nilikueleza njia zangu ukanijibu,
nifundishe sheria zako.

---

[a]**119:2** Za 40:16; 112:1; 119:146; Isa 56:2; Kum 10:12; Mit 9:7; 1Nya 16:11
[b]**119:3** Za 59:4; 128:1; Yn 3:9; 5:18; Yer 6:16; 7:23; Rum 7:16, 17
[c]**119:4** Za 103:18; 119:56; Kum 6:17
[d]**119:5** Law 19:37; Yer 31:33; 2Kor 3:5; Rum 7:22, 23
[e]**119:6** Za 119:46, 80, 117; Ay 22:26; 1Yn 2:28
[f]**119:7** Kum 4:8
[g]**119:7** Za 90:13; 103:13; 119:47
[h]**119:8** Za 38:21
[i]**119:9** Za 119:65, 169; 39:1; Mit 1:4, 10
[j]**119:10** Za 119:21, 118; 9:1; 2Nya 15:15
[k]**119:11** Isa 63:13; Mit 3:23; Za 119:133, 165; 18:22-23; Kum 6:6; Lk 2:19; Ay 22:22
[l]**119:12** Isa 63:13; Lk 2:19
[m]**119:13** Za 119:72
[n]**119:14** Za 119:111
[o]**119:15** Za 119:97, 148; 1:2
[p]**119:16** Za 112:1
[q]**119:17** Za 13:6; 116:7; 119:67; 103:20
[r]**119:19** Mwa 23:4; Ebr 11:13
[s]**119:20** Za 84:2; 119:131; 42:2; 63:1; Isa 26:9
[t]**119:21** Za 119:10, 51; 5:5; Ay 30:1; Yer 20:7; 50:32; Kum 27:26; Dan 4:37; Mal 3:15
[u]**119:22** Za 39:8; 119:2
[v]**119:25** Za 44:25; 143:11; 119:9, 50, 107
[w]**119:26** Za 25:4; 27:11; 86:11; 1Fal 8:36

27 [a]Nijulishe mafundisho ya mausia
yako,
nami nitatafakari maajabu yako.
28 [b]Nafsi yangu imechakazwa kwa
huzuni,
uniimarishe sawasawa na neno
lako.
29 [c]Niepushe na njia za udanganyifu,
kwa neema unifundishe sheria
zako.
30 [d]Nimechagua njia ya kweli,
nimekaza moyo wangu katika
sheria zako.
31 [e]Nimeng'ang'ania sheria zako, Ee
Bwana,
usiniache niaibishwe.
32 [f]Nakimbilia katika njia ya maagizo
yako,
kwa kuwa umeuweka moyo
wangu huru.

*Maombi Ili Kupata Ufahamu Wa Sheria*

33 [g]Ee Bwana, nifundishe kuyafuata
maagizo yako,
nami nitayashika mpaka mwisho.
34 [h]Nipe ufahamu, nami nitaishika
sheria yako
na kuitii kwa moyo wangu wote.
35 [i]Niongoze kwenye njia ya amri zako,
kwa kuwa huko napata furaha.
36 [j]Ugeuze moyo wangu kuelekea
sheria zako,
na siyo kwenye mambo ya
ubinafsi.
37 [k]Geuza macho yangu kutoka kwenye
mambo yasiyofaa,
uyahifadhi maisha yangu
sawasawa na neno lako.
38 [l]Mtimizie mtumishi wako ahadi
yako,
ili upate kuogopwa.
39 [m]Niondolee aibu ninayoiogopa,
kwa kuwa sheria zako ni njema.
40 [n]Tazama jinsi ninavyoonea shauku
mausia yako!
Hifadhi maisha yangu katika haki
yako.

*Kuitumainia Sheria Ya Bwana*

41 [o]Ee Bwana, upendo wako usiokoma
unijie,
wokovu wako sawasawa na ahadi
yako,
42 [p]ndipo nitakapomjibu
anayenidhihaki,
kwa kuwa ninalitumainia neno
lako.
43 [q]Usilinyakue neno la kweli kutoka
kinywani mwangu,
kwa kuwa nimeweka tumaini
langu katika amri zako.
44 [r]Nitaitii amri yako daima,
naam, milele na milele.
45 [s]Nitatembea nikiwa huru,
kwa kuwa nimejifunza mausia
yako.
46 [t]Nitasema sheria zako mbele za
wafalme
wala sitaaibishwa,
47 [u]kwa kuwa ninazifurahia amri zako
kwa sababu ninazipenda.

---

[a]**119:27** Za 105:2; 145:5
[b]**119:28** Za 119:9; 116:3; 18:1; 6:7; Yer 45:3; Isa 51:11; 40:29; 41:10
[c]**119:29** Za 26:4; Hes 6:25; Mit 30:8; Ebr 8:10
[d]**119:30** Yos 24:22; Za 26:3; 108:1
[e]**119:31** Kum 10:20
[f]**119:32** 1Fal 4:29; Isa 60:5; 2Kor 6:11
[g]**119:33** Za 119:12
[h]**119:34** Za 119:27, 69, 73, 144, 169; Mit 2:6; Ay 32:8; Yak 1:5; Kum 6:25; Dan 2:21
[i]**119:35** Za 119:32; 1:2; 25:4, 5
[j]**119:36** Yos 24:23; Ebr 13:5; Mk 7:21; 12:15; Eze 33:31; 1Tim 6:10
[k]**119:37** Za 119:9, 25; 71:20; Ay 31:1
[l]**119:38** Hes 23:19; 2Sam 7:25
[m]**119:39** Za 119:22; 69:9; 89:51; Isa 25:8; 51:7; 54:4
[n]**119:40** Za 119:20, 25, 149, 154
[o]**119:41** Za 6:4; 119:76, 116, 154, 170
[p]**119:42** Mit 27:11; Za 42:10
[q]**119:43** Za 119:74, 81, 114, 147; 1Fal 17:24
[r]**119:44** Za 119:33, 34, 55; Kum 6:25
[s]**119:45** Za 119:94, 155; Yn 8:32, 36; Rum 8:2
[t]**119:46** Mt 10:18; Mdo 26:1, 2; Za 119:6
[u]**119:47** Za 119:77, 97, 127, 143, 159, 163, 165

48 [a]Ninaziinulia amri zako ambazo
ninazipenda mikono yangu,
nami ninatafakari juu ya maagizo
yako.

*Matumaini Katika Sheria Ya Bwana*

49 [b]Kumbuka neno lako kwa mtumishi
wako,
kwa sababu umenipa tumaini.
50 [c]Faraja yangu katika mateso yangu
ni hii:
Ahadi yako inahifadhi maisha
yangu.
51 [d]Wenye majivuno wamenisimanga
bila kuchoka,
hata hivyo sitaiacha sheria yako.
52 [e]Ee Bwana, ninazikumbuka sheria
zako za zamani,
nazo zinanifariji.
53 [f]Nimeshikwa sana na ghadhabu kwa
ajili ya waovu,
ambao wameacha sheria yako.
54 [g]Maagizo yako ni kiini cha nyimbo
zangu
popote ninapoishi.
55 [h]Ee Bwana, wakati wa usiku
ninalikumbuka jina lako,
nami nitatii sheria yako.
56 [i]Hili limekuwa zoezi langu:
nami ninayatii mausia yako.

*Kujitolea Katika Sheria Ya Bwana*

57 [j]Ee Bwana, wewe ni fungu langu,
nimeahidi kuyatii maneno yako.
58 [k]Nimetafuta uso wako kwa moyo
wangu wote,
nihurumie sawasawa na ahadi
yako.
59 [l]Nimezifikiri njia zangu
na nimeelekeza hatua zangu
katika mausia yako.
60 [m]Nitafanya haraka bila kuchelewa
kuzitii amri zako.
61 [n]Hata waovu wanifunge kwa kamba,
sitasahau sheria yako.
62 [o]Usiku wa manane ninaamka
kukushukuru
kwa sababu ya sheria zako za
haki.
63 [p]Mimi ni rafiki kwa wale wote
wakuchao,
kwa wote wanaofuata mausia
yako.
64 [q]Ee Bwana, dunia imejaa upendo
wako,
nifundishe maagizo yako.

*Thamani Ya Sheria Ya Bwana*

65 [r]Mtendee wema mtumishi wako
Ee Bwana, sawasawa na neno
lako.
66 [s]Nifundishe maarifa na uamuzi
mzuri,
kwa kuwa ninaamini amri zako.
67 [t]Kabla sijapata shida nilipotea njia,
lakini sasa ninalitii neno lako.
68 [u]Wewe ni mwema, unalotenda ni
jema,
nifundishe maagizo yako.

---

[a]**119:48** Mwa 24:63
[b]**119:49** Za 119:9, 43
[c]**119:50** Za 119:25; 27:13; Yer 15:16; Rum 5:3-5; Ebr 6:17-19
[d]**119:51** Za 119:21; Ay 16:10; 17:2; 23:11; Yer 20:7
[e]**119:52** Za 103:18
[f]**119:53** Kut 32:19; 33:4; Za 89:30; Ezr 9:3
[g]**119:54** Za 119:172; 101:1; 138:5
[h]**119:55** Za 119:44, 62, 72; 1:2; 42:8; 63:6; 77:2; Isa 26:9; Mdo 16:25
[i]**119:56** Za 119:4, 100, 134; Hes 15:40
[j]**119:57** Kum 32:9; Yer 51:19; Za 119:17, 67, 101; Mao 3:24
[k]**119:58** Kum 4:29; Ezr 9:8; 1Nya 16:11; Za 34:4; 119:41; Mwa 43:29
[l]**119:59** Yoe 2:13; Lk 15:17; Yos 24:14, 15
[m]**119:60** Za 119:115
[n]**119:61** Za 119:83, 109, 153, 176
[o]**119:62** Za 119:55; 119:7; Mdo 16:25
[p]**119:63** Za 15:4; 101:6, 7; 103:11; 119:56; 111:10
[q]**119:64** Za 33:5; 119:12, 108
[r]**119:65** Isa 50:2; 59:1; Za 119:9, 17; 125:4; Mik 2:7
[s]**119:66** Za 51:6
[t]**119:67** Za 116:10; 95:10; 119:17; Ebr 12:11; Yer 8:4; 31:18; Kum 32:15; Ufu 3:19
[u]**119:68** Za 100:5; 106:1; 107:1; 135:3; Kut 18:20; 34:6; Mt 19:17

69 [a]Ingawa wenye majivuno
wamenisingizia uongo,
nitafuata mausia yako kwa moyo
wangu wote.
70 [b]Mioyo yao ni katili na migumu,
bali mimi napendezwa na sheria
yako.
71 [c]Ilikuwa vyema mimi kupata shida
ili nipate kujifunza maagizo yako.
72 [d]Sheria inayotoka kinywani mwako
ina thamani kubwa kwangu
kuliko maelfu ya vipande vya
fedha na dhahabu.

*Haki Ya Sheria Ya Bwana*

73 [e]Mikono yako ilinifanya na
kuniumba,
nipe ufahamu niweze kujifunza
amri zako.
74 [f]Wakuchao wafurahie wanaponiona,
kwa kuwa nimeweka tumaini
langu katika neno lako.
75 [g]Ee Bwana, ninajua kwamba sheria
zako ni za haki,
katika uaminifu wako
umeniadhibu.
76 [h]Upendo wako usiokoma uwe faraja
yangu,
sawasawa na ahadi yako kwa
mtumishi wako.
77 Huruma yako na inijie ili nipate
kuishi,
kwa kuwa naifurahia sheria yako.
78 [i]Wenye majivuno na waaibishwe
kwa kunikosea mimi bila
sababu,
lakini mimi nitatafakari juu ya
mausia yako.
79 [j]Wale wakuchao na wanigeukie
mimi,
hao ambao wanazielewa sheria
zako.
80 [k]Moyo wangu usiwe na lawama
katika kutii maagizo yako,
ili nisiaibishwe.

*Maombi Kwa Ajili Ya Kuokolewa*

81 [l]Nafsi yangu inazimia kwa kutamani
wokovu wako,
lakini nimeweka tumaini langu
katika neno lako.
82 [m]Macho yangu yamefifia, nikingoja
ahadi yako;
ninasema, “Utanifajiri lini?”
83 [n]Ingawa nimekuwa kama kiriba
kwenye moshi,
bado sijasahau maagizo yako.
84 Mtumishi wako itampasa angoje
mpaka lini?
Ni lini utawaadhibu washtaki
wangu?
85 [o]Wenye majivuno wananichimbia
mashimo,
kinyume na sheria yako.
86 [p]Amri zako zote ni za kuaminika;
unisaidie, kwa sababu watu
wananishtaki bila sababu.
87 [q]Walikaribia kabisa kunifuta kutoka
uso wa dunia,
lakini sijaacha mausia yako.
88 [r]Yahifadhi maisha yangu sawasawa
na upendo wako,
nami nitatii sheria za kinywa
chako.

---

[a]**119:69** Ay 13:4; Za 109:2
[b]**119:70** Mdo 28:27; Za 17:10; Isa 29:13
[c]**119:71** Za 119:67, 75; Ebr 12:10
[d]**119:72** Ay 28:17; Za 19:10; Mt 8:10
[e]**119:73** Mwa 1:27; Ay 4:17; 10:8; Za 139:13-16; 100:3; 138:8
[f]**119:74** Za 34:2; 119:9; 130:5
[g]**119:75** Za 89:30, 31; 119:7, 138, 172; Ebr 12:5-11
[h]**119:76** Za 6:4; 119:41
[i]**119:78** Za 119:51; 35:19; 119:86, 161; 25:3; Yer 50:32
[j]**119:79** Za 119:27, 125
[k]**119:80** Za 119:1; 119:6; 1Fal 8:61; Mwa 26:5
[l]**119:81** Za 119:20, 43, 123; 84:2; 73:26
[m]**119:82** Mao 2:11; Za 6:7; 69:3; 119:41, 123
[n]**119:83** Za 119:61; 119:84; Ay 30:30; Ufu 6:10; Yer 12:3; 15:15; 20:11; Za 39:4; 6:3; 119:51; 7:6
[o]**119:85** Za 35:7; 119:51; 57:6; Yer 18:20, 22
[p]**119:86** Za 109:26; 7:1-5; 35:19; 119:78, 138
[q]**119:87** Isa 1:4, 28; 59:13; 58:2; Za 119:150
[r]**119:88** Za 41:2; 119:2, 100, 124, 129, 134, 168; 51:1; 109:26

*Imani Katika Sheria Ya Bwana*

89 [a]Ee Bwana, neno lako ni la milele,
linasimama imara mbinguni.
90 [b]Uaminifu wako unaendelea kwa vizazi vyote,
umeiumba dunia, nayo inadumu.
91 [c]Sheria zako zinadumu hadi leo,
kwa kuwa vitu vyote vinakutumikia.
92 [d]Kama nisingefurahia sheria yako,
ningeangamia katika taabu zangu.
93 [e]Sitasahau mausia yako kamwe,
kwa maana kwayo umehifadhi maisha yangu.
94 [f]Uniokoe, kwa maana mimi ni wako,
kwa kuwa nimetafuta mausia yako.
95 [g]Waovu wanangojea kuniangamiza,
bali mimi ninatafakari sheria zako.
96 [h]Katika ukamilifu wote ninaona mna kikomo,
lakini amri zako hazina mpaka.

*Kuipenda Sheria Ya Bwana*

97 [i]Aha! Tazama, sheria yako naipenda mno ajabu.
Ninaitafakari mchana kutwa.
98 [j]Amri zako zimenipa hekima zaidi kuliko adui zangu,
kwa kuwa nimezishika daima.
99 [k]Nina akili zaidi kuliko walimu wangu wote,
kwa kuwa ninatafakari juu ya sheria zako.
100 [l]Nina ufahamu zaidi kuliko wazee,
kwa kuwa ninayatii mausia yako.
101 [m]Nimezuia miguu yangu isiende kwenye kila njia mbaya,
ili niweze kutii neno lako.
102 [n]Sijaziacha sheria zako,
kwa kuwa umenifundisha wewe mwenyewe.
103 [o]Tazama jinsi maneno yako yalivyo matamu kwangu,
matamu kuliko asali katika kinywa changu!
104 [p]Ninapata ufahamu kutoka mausia yako,
kwa hiyo ninachukia kila njia ya upotovu.

*Nuru Kutoka Kwenye Sheria Ya Bwana*

105 [q]Neno lako ni taa ya miguu yangu
na mwanga katika njia yangu.
106 [r]Nimeapa na nimethibitisha,
kwamba nitafuata sheria zako za haki.
107 [s]Nimeteseka sana, uhifadhi maisha yangu, Ee Bwana,
sawasawa na neno lako.
108 [t]Ee Bwana, pokea sifa za hiari za kinywa changu,
nifundishe sheria zako.
109 [u]Ingawa maisha yangu yako hatarini siku zote,
sitasahau sheria yako.

---

[a]**119:89** Za 119:111, 144; 111:8; Isa 51:6; Mt 5:18; 1Pet 1:25
[b]**119:90** Za 36:5; 45:17; 148:6; Ay 8:19
[c]**119:91** Yer 33:25; 31:35; Za 148:6; 104:2-4; Mwa 8:22
[d]**119:92** Za 37:4, 5; 112:1; 119:50, 67; Rum 15:4
[e]**119:93** Za 119:83; 103:5
[f]**119:94** Za 119:45, 146; 54:1; 116:4; Yer 17:14; 31:18; 42:11; Hos 2:7, 16
[g]**119:95** Za 69:4; 119:99
[h]**119:96** Za 19:7; Isa 40:8; Mt 5:18
[i]**119:97** Za 1:2; 119:15, 47
[j]**119:98** 2Tim 3:17; Kum 4:6, 8; 19:7; Isa 48:17
[k]**119:99** 2Tim 3:15; Za 119:15
[l]**119:100** Ay 12:12; 32:7; Za 119:56; Kum 6:17
[m]**119:101** Mit 1:15; 2Kor 7:1; Za 119:57
[n]**119:102** Kum 17:20; 4:5
[o]**119:103** Mit 24:13, 14; 8:11; Za 19:10
[p]**119:104** Za 111:10; 119:7
[q]**119:105** Mit 6:23; 20:27; 2Pet 1:19; Za 119:130
[r]**119:106** Neh 10:29; Za 119:7
[s]**119:107** Za 119:25
[t]**119:108** Za 51:15; 109:30; 63:5; 119:64; 71:8; Ebr 13:15; Hos 14:2
[u]**119:109** Amu 12:3; Za 119:61; Ay 13:14

110 [a]Waovu wamenitegea mtego,
lakini sijayakiuka maagizo yako.
111 [b]Sheria zako ni urithi wangu milele,
naam ni furaha ya moyo wangu.
112 [c]Nimekusudia moyoni mwangu
kuyafuata maagizo yako mpaka mwisho.

*Usalama Ndani Ya Sheria Ya Bwana*

113 [d]Ninachukia watu wa nia mbili,
lakini ninapenda sheria yako.
114 [e]Wewe ni kimbilio langu na ngao yangu,
nimeweka tumaini langu katika neno lako.
115 [f]Ondokeni kwangu, ninyi mtendao mabaya,
ili niweze kushika amri za Mungu wangu!
116 [g]Nihifadhi sawasawa na ahadi yako, nami nitaishi;
usiache matumaini yangu yakavunjwa.
117 [h]Nitegemeze, nami nitaokolewa,
nami daima nitayaheshimu maagizo yako.
118 [i]Unawakataa wote wanaoyaasi maagizo yako,
kwa maana udanganyifu wao ni bure.
119 [j]Waovu wa nchi unawatupa kama takataka,
kwa hivyo nazipenda sheria zako.
120 [k]Mwili wangu unatetemeka kwa kukuogopa wewe,
ninaziogopa sheria zako.

*Kuitii Sheria Ya Bwana*

121 [l]Nimetenda yaliyo haki na sawa,
usiniache mikononi mwa watesi wangu.
122 [m]Mhakikishie mtumishi wako usalama,
usiache wenye kiburi wanionee.
123 [n]Macho yangu yamefifia, yakitazamia wokovu wako,
na kuitazamia ahadi yako ya kweli.
124 [o]Mfanyie mtumishi wako kulingana na upendo wako
na unifundishe maagizo yako.
125 [p]Mimi ni mtumishi wako; nipe ufahamu
ili niweze kuelewa sheria zako.
126 [q]Ee Bwana, wakati wako wa kutenda umewadia,
kwa kuwa sheria yako inavunjwa.
127 [r]Kwa sababu nazipenda amri zako zaidi ya dhahabu,
naam, zaidi ya dhahabu safi,
128 [s]na kwa sababu naona maagizo yako yote ni adili,
nachukia kila njia potovu.

*Shauku Ya Kuitii Sheria Ya Bwana*

129 [t]Sheria zako ni za ajabu,
hivyo ninazitii.

[a]**119:110** Za 25:15; 64:5; 119:10; Isa 8:14; Amo 3:5
[b]**119:111** Kum 33:4; Za 119:14, 162
[c]**119:112** Za 108:1; 119:33
[d]**119:113** 1Fal 18:21; Yak 1:8; 4:8; Za 119:47
[e]**119:114** Za 18:2; 119:43; 32:7; Mwa 15:1
[f]**119:115** Za 6:8; Mt 7:23
[g]**119:116** Za 18:35; 41:3; 55:22; 119:41; Isa 46:4; Rum 5:5; 9:33
[h]**119:117** Isa 41:10; 46:4; Za 34:4; 119:6; 71:6; Yn 10:28; Rum 14:4
[i]**119:118** Za 119:10
[j]**119:119** Isa 1:22, 25; Eze 18:19; Za 119:47
[k]**119:120** Ay 4:14
[l]**119:121** 2Sam 8:15; Ay 27:6
[m]**119:122** Ay 17:3
[n]**119:123** Isa 38:14; Za 119:81, 82
[o]**119:124** Za 119:12, 88; 25:7
[p]**119:125** Za 116:16; 119:79
[q]**119:126** Hes 15:31
[r]**119:127** Efe 3:8; Za 19:10; 119:47; Ay 3:21; Mit 3:13, 18; 8:11
[s]**119:128** Za 19:8; 31:6; 119:104, 163; Mit 13:5
[t]**119:129** Za 119:18, 22, 88

130 [a]Kuingia kwa maneno yako
kunaleta nuru,
kunampa mjinga ufahamu.
131 [b]Nimefungua kinywa changu
na kuhema,
nikitamani amri zako.
132 [c]Nigeukie na unihurumie,
kama uwafanyiavyo siku zote
wale wanaolipenda jina lako.
133 [d]Ongoza hatua zangu
kulingana na neno lako,
usiache dhambi yoyote initawale.
134 [e]Niokoe na uonevu wa
wanadamu,
ili niweze kutii mausia yako.
135 [f]Mwangazie mtumishi wako
uso wako
na unifundishe amri zako.
136 [g]Chemchemi za machozi
zinatiririka kutoka machoni
yangu,
kwa kuwa sheria yako haifuatwi.

*Haki Ya Sheria Ya Bwana*

137 [h]Ee Bwana, wewe ni mwenye
haki,
sheria zako ni sahihi.
138 [i]Sheria ulizoziweka ni za haki,
ni za kuaminika kikamilifu.
139 [j]Jitihada yangu
imenidhoofisha, kwa kuwa
adui zangu
wanayapuuza maneno yako.
140 [k]Ahadi zako zimejaribiwa
kikamilifu,
mtumishi wako anazipenda.
141 [l]Ingawa ni mdogo na
ninadharauliwa,
sisahau mausia yako.
142 [m]Haki yako ni ya milele,
na sheria yako ni kweli.
143 [n]Shida na dhiki zimenipata,
lakini amri zako ni furaha yangu.
144 [o]Sheria zako ni sahihi milele,
hunipa ufahamu ili nipate kuishi.

*Maombi Kwa Ajili Ya Kuokolewa*

145 [p]Ee Bwana, ninakuita kwa
moyo wangu wote,
nami nitayatii maagizo yako.
146 [q]Ninakuita; niokoe
nami nitazishika sheria zako.
147 [r]Ninaamka asubuhi na
mapema na kukuomba
msaada;
nimeweka tumaini langu katika
neno lako.
148 [s]Sikufumba macho yangu
usiku kucha,
ili niweze kutafakari juu ya ahadi
zako.
149 [t]Usikie sauti yangu sawasawa
na upendo wako,
Ee Bwana, uyahifadhi maisha
yangu, sawasawa na sheria
zako.
150 [u]Wale wanaopanga mipango
miovu wako karibu nami,
lakini wako mbali na sheria yako.

---

[a]**119:130** Za 119:105; 19:7, 10; Mit 1:4; 2Pet 1:19
[b]**119:131** Za 42:1; 119:20
[c]**119:132** 2Sam 24:14; Kut 4:31; Za 6:4; 9:13; 5:11; 106:4; 1Sam 1:11
[d]**119:133** Kum 6:12; Za 119:9, 11, 122; Rum 6:16
[e]**119:134** Lk 1:74; Za 119:56, 88, 122
[f]**119:135** Hes 6:25; Za 4:6; 80:3; 4:6; 119:12
[g]**119:136** Yer 9:1; 9:1, 18; 13:17; 14:17; Mao 1:16; 3:48; Isa 22:4; 42:24; Eze 9:4; Za 6:6; 119:158; 106:25
[h]**119:137** Kut 9:27; Ezr 9:15; Neh 9:13, 33; Yer 12:1; Dan 9:7
[i]**119:138** Za 119:75, 86; 19:7
[j]**119:139** Za 69:9; Yn 2:17
[k]**119:140** Yos 23:14; Za 12:6; 119:47
[l]**119:141** Za 22:6; 119:61, 134; Mit 15:16; Amo 7:2; Lk 6:20; 2Kor 8:9; Yak 2:5
[m]**119:142** Za 119:151, 160; 19:7, 9; Yn 17:17; Efe 1:3
[n]**119:143** Za 119:24, 47
[o]**119:144** Za 119:34
[p]**119:145** Za 119:10, 22, 55
[q]**119:146** Za 119:94
[r]**119:147** Za 3:3; 57:8; 108:2
[s]**119:148** Za 63:6; 63:1, 6
[t]**119:149** Za 27:7; 124; 119:40
[u]**119:150** Za 37:7

151 [a]Ee Bwana, hata hivyo wewe u karibu,
na amri zako zote ni za kweli.
152 [b]Tangu zamani nimejifunza kutoka shuhuda zako
kwamba umezithibitisha ili zidumu milele.

*Maombi Kwa Ajili Ya Msaada*

153 [c]Yaangalie mateso yangu, uniokoe,
kwa kuwa sijasahau sheria yako.
154 [d]Nitetee katika hali hii yangu na unikomboe,
uyahifadhi maisha yangu sawasawa na ahadi yako.
155 [e]Wokovu uko mbali na waovu,
kwa kuwa hawatafuti maagizo yako.
156 [f]Ee Bwana, huruma zako ni kuu,
uyahifadhi maisha yangu sawasawa na sheria zako.
157 [g]Adui wanaonitesa ni wengi,
lakini mimi sitaziacha sheria zako.
158 [h]Ninawatazama wasioamini kwa chuki,
kwa kuwa hawalitii neno lako.
159 [i]Tazama jinsi ninavyopenda mausia yako;
Ee Bwana, uyahifadhi maisha yangu, sawasawa na upendo wako.
160 [j]Maneno yako yote ni kweli,
sheria zako zote za haki ni za milele.

*Kujiweka Wakfu Kwa Sheria Ya Bwana*

161 [k]Watawala wamenitesa bila sababu,
lakini moyo wangu unatetemeka kwa neno lako.
162 [l]Nafurahia ahadi zako
kama mtu aliyepata mateka mengi.
163 Ninachukia na kuchukizwa sana na uongo,
lakini napenda sheria yako.
164 [m]Ninakusifu mara saba kwa siku,
kwa ajili ya sheria zako za haki.
165 [n]Wanaopenda sheria yako wana amani tele,
wala hakuna kitu kinachoweza kuwakwaza.
166 [o]Ee Bwana, ninangojea wokovu wako,
nami ninafuata amri zako,
167 [p]Ninazitii sheria zako,
kwa sababu ninazipenda mno.
168 [q]Nimetii mausia yako na sheria zako,
kwa kuwa njia zangu zote zinajulikana kwako.

*Kuomba Msaada*

169 [r]Ee Bwana, kilio changu na kifike mbele zako,
nipe ufahamu sawasawa na neno lako.
170 [s]Maombi yangu na yafike mbele zako,
niokoe sawasawa na ahadi yako.

---

[a]**119:151** Flp 4:5; Za 34:18; 119:142; 145:18
[b]**119:152** Za 119:7, 73, 89; 111:8; Lk 21:33
[c]**119:153** Za 13:3; 3:7; 44:17; Mao 5:1
[d]**119:154** Za 119:24, 41; 35:1; 1Sam 24:15; Yer 50:34; Mik 7:9
[e]**119:155** Za 119:94, 118; Ay 5:4
[f]**119:156** Neh 9:27; Yak 5:11; Za 119:25, 149
[g]**119:157** Za 7:1; 44:18
[h]**119:158** Za 119:104, 136; Kut 32:19
[i]**119:159** Za 119:25; 41:2
[j]**119:160** Za 119:89; 111:8
[k]**119:161** Za 119:23, 122, 157; 119:120; 1Sam 24:14-15
[l]**119:162** Za 119:25; 41:2
[m]**119:164** Za 119:111; 1Sam 30:16; Isa 9:3; 53:12
[n]**119:165** Za 119:11; 37:11; 37:24; Isa 26:3, 12; 27:5; 32:17; 57:19; 66:12; 1Yn 2:10; Mit 3:2
[o]**119:166** Za 119:81
[p]**119:167** Za 119:47
[q]**119:168** Za 139:3; Ay 10:4; 23:10; Mit 5:21
[r]**119:169** Ay 16:18; Za 119:9, 34
[s]**119:170** 1Fal 8:30; 2Nya 6:24; Za 28:2; 140:6; 143:1; 3:7; 22:20; 59:1; 119:41

171 [a]Midomo yangu na ibubujike
sifa,
kwa kuwa unanifundisha maagizo
yako.
172 [b]Ulimi wangu na uimbe
kuhusu neno lako,
kwa kuwa amri zako zote ni za
haki.
173 [c]Mkono wako uwe tayari
kunisaidia,
kwa kuwa nimechagua mausia
yako.
174 [d]Ee BWANA, ninatamani
wokovu wako,
na sheria yako ni furaha yangu.
175 [e]Nijalie kuishi ili nipate
kukusifu,
na sheria zako zinitegemeze.
176 [f]Nimetangatanga kama
kondoo aliyepotea.
Mtafute mtumishi wako,
kwa kuwa sijasahau amri zako.

## Zaburi 120

*Kuomba Msaada*

*Wimbo wa kwenda juu.*

1 [g]Katika dhiki yangu namwita
BWANA,
naye hunijibu.
2 [h]Ee BWANA, uniokoe kutoka midomo
ya uongo
na ndimi za udanganyifu.

3 Atakufanyia nini,
au akufanyie nini zaidi, ewe ulimi
mdanganyifu?
4 [i]Atakuadhibu kwa mishale mikali ya
shujaa,
kwa makaa yanayowaka ya mti wa
mretemu.

5 [j]Ole wangu kwa kuwa naishi
Mesheki,
kwamba naishi katikati ya hema
za Kedari!
6 Nimeishi muda mrefu mno
miongoni mwa wale wanaochukia
amani.
7 Mimi ni mtu wa amani;
lakini ninaposema, wao wanataka
vita.

## Zaburi 121

*BWANA Mlinzi Wetu*

*Wimbo wa kwenda juu.*

1 Nayainua macho yangu nitazame
vilima,
msaada wangu utatoka wapi?
2 [k]Msaada wangu hutoka kwa BWANA,
Muumba wa mbingu na dunia.

3 [l]Hatauacha mguu wako uteleze,
yeye akulindaye hatasinzia,
4 [m]hakika, yeye alindaye Israeli
hatasinzia wala hatalala usingizi.
5 [n]BWANA anakulinda,
BWANA ni uvuli wako mkono
wako wa kuume,
6 [o]jua halitakudhuru mchana,
wala mwezi wakati wa usiku.
7 [p]BWANA atakukinga na madhara
yote,
atayalinda maisha yako,
8 [q]BWANA atakulinda unapoingia na
unapotoka,
tangu sasa na hata milele.

---

[a]**119:171** Za 51:15; 63:3; 94:12; Isa 2:3; Mik 4:2
[b]**119:172** Za 51:14; 119:7, 75
[c]**119:173** Za 37:24; 73:23; Isa 41:10; Lk 10:42; Yos 24:22; Mit 1:29
[d]**119:174** Za 119:16, 24, 166
[e]**119:175** Za 119:116, 159; Isa 55:3
[f]**119:176** Za 119:10; 95:10; Yer 50:17; Eze 34:11; Lk 15:4
[g]**120:1** 2Sam 22:7; Za 18:1; 118:5
[h]**120:2** Za 31:18; 52:4
[i]**120:4** Kum 32:23
[j]**120:5** Mwa 25:13; 2:10; Yer 2:10; 49:28; 1Sam 25:1
[k]**121:2** Mwa 1:1; Za 104:5
[l]**121:3** 1Sam 2:9; Isa 27:3
[m]**121:4** Za 127:1
[n]**121:5** Za 1:6
[o]**121:6** Isa 49:10
[p]**121:7** Za 9:9, 10; 91:9, 10; Ay 5:19; Mit 12:21
[q]**121:8** Kum 28:6; Mit 2:8

## Zaburi 122

*Sifa Kwa Yerusalemu*

*Wimbo wa kwenda juu. Wa Daudi.*

1 [a]Nilishangilia pamoja na wale
walioniambia,
"Twende nyumbani ya BWANA."
2 Ee Yerusalemu, miguu yetu
imesimama
malangoni mwako.

3 [b]Yerusalemu imejengwa vyema kama
mji
ambao umeshikamanishwa
pamoja.
4 [c]Huko ndiko makabila hukwea,
makabila ya BWANA,
kulisifu jina la BWANA kulingana na
maagizo
waliopewa Israeli.
5 Huko viti vya enzi vya hukumu
hukaa,
viti vya enzi vya nyumba ya
Daudi.

6 [d]Omba kwa ajili ya amani ya
Yerusalemu:
"Wote wakupendao na wawe
salama.
7 [e]Amani na iwepo ndani ya kuta zako
na usalama ndani ya ngome zako."
8 Kwa ajili ya ndugu zangu na
marafiki,
nitasema, "Amani iwe ndani
yako."
9 [f]Kwa ajili ya nyumba ya BWANA
Mungu wetu,
nitatafuta mafanikio yako.

## Zaburi 123

*Kuomba Rehema*

*Wimbo wa kwenda juu.*

1 [g]Ninayainua macho yangu kwako,
kwako wewe ambaye kiti chako
cha enzi kiko mbinguni.
2 [h]Kama vile macho ya watumwa
yatazamavyo mkono wa bwana
wao,
kama vile macho ya mtumishi wa
kike
yatazamavyo mkono wa bibi yake,
ndivyo macho yetu yamtazamavyo
BWANA Mungu wetu,
mpaka atakapotuhurumia.

3 Uturehemu, Ee BWANA, uturehemu,
kwa maana tumevumilia dharau
nyingi.
4 Tumevumilia dhihaka nyingi kutoka
kwa wenye kiburi,
dharau nyingi kutoka kwa wenye
majivuno.

## Zaburi 124

*Shukrani Kwa Ukombozi Wa Israeli*

*Wimbo wa kwenda juu. Wa Daudi.*

1 [i]Kama BWANA asingalikuwa upande
wetu;
Israeli na aseme sasa:
2 kama BWANA asingalikuwa upande
wetu,
wakati watu walipotushambulia,
3 [j]wakati hasira yao ilipowaka dhidi
yetu,
wangalitumeza tungali hai,
4 [k]mafuriko yangalitugharikisha,
maji mengi yangalitufunika,
5 maji yaendayo kasi
yangalituchukua.

6 BWANA asifiwe,
yeye ambaye hakuruhusu
turaruliwe kwa meno yao.
7 [l]Tumeponyoka kama ndege
kutoka mtego wa mwindaji;
mtego umevunjika,
nasi tukaokoka.

---

[a] **122:1** Isa 49:10; Yer 31:6; Zek 8:21
[b] **122:3** 2Sam 5:9; Efe 2:21
[c] **122:4** Kum 16:16; Kut 16:34
[d] **122:6** Za 26:8; Isa 62:6; Yer 51:50
[e] **122:7** 1Sam 25:6; Za 48:3
[f] **122:9** Za 128:5
[g] **123:1** Za 68:5; Isa 6:1; 63:15
[h] **123:2** Za 25:15
[i] **124:1** Za 129:1; Mwa 15:1; Hes 14:9; Yos 1:5
[j] **124:3** Za 35:25; Mit 1:12; Yer 51:34
[k] **124:4** Za 88:17; 18:4
[l] **124:7** Za 91:3; 25:15

8 [a]Msaada wetu ni katika jina la BWANA,
Muumba wa mbingu na dunia.

## Zaburi 125

*Usalama Wa Watu Wa Mungu*

*Wimbo wa kwenda juu.*

1 [b]Wale wamtumainio BWANA ni kama mlima Sayuni,
ambao hauwezi kutikisika, bali wadumu milele.
2 [c]Kama milima inavyozunguka Yerusalemu,
ndivyo BWANA anavyowazunguka watu wake
sasa na hata milele.

3 [d]Fimbo ya waovu haitadumu juu ya nchi
waliopewa wenye haki,
ili wenye haki wasije wakatumia
mikono yao kutenda ubaya.

4 [e]Ee BWANA, watendee mema walio wema,
wale walio wanyofu wa moyo.
5 [f]Bali wale wanaogeukia njia zilizopotoka,
BWANA atawafukuza pamoja na watenda mabaya.

Amani iwe juu ya Israeli.

## Zaburi 126

*Kurejezwa Kutoka Utumwani*

*Wimbo wa kwenda juu.*

1 [g]BWANA alipowarejeza mateka Sayuni,
tulikuwa kama watu walioota ndoto.
2 [h]Vinywa vyetu vilijaa kicheko,
ndimi zetu zilijaa nyimbo za shangwe.
Ndipo iliposemwa miongoni mwa mataifa,
"BWANA amewatendea mambo makuu."
3 [i]BWANA ametutendea mambo makuu,
nasi tumejaa furaha.

4 [j]Ee BWANA, turejeshee watu wetu waliotekwa,
kama vijito katika Negebu.
5 [k]Wapandao kwa machozi
watavuna kwa nyimbo za shangwe.
6 Yeye azichukuaye mbegu zake
kwenda kupanda, huku akilia,
atarudi kwa nyimbo za shangwe,
akichukua miganda ya mavuno yake.

## Zaburi 127

*Bila Mungu, Kazi Ya Mwanadamu Haifai*

*Wimbo wa kwenda juu. Wa Solomoni.*

1 [l]BWANA asipoijenga nyumba,
wajengao hufanya kazi bure.
BWANA asipoulinda mji,
walinzi wakesha bure.
2 [m]Mnajisumbua bure kuamka mapema
na kuchelewa kulala,
mkitaabikia chakula:
kwa maana yeye huwapa usingizi wapenzi wake.

3 [n]Wana ni urithi utokao kwa BWANA,
watoto ni zawadi kutoka kwake.

---

[a]**124:8** 1Sam 17:45; Mwa 1:1; Za 115:15; 121:2; 134:3; Kut 18:4; Mit 18:10; Isa 50:10
[b]**125:1** Za 46:5; 48:2-5; 48:12; Isa 33:20
[c]**125:2** 1Nya 21:15; Za 32:10; Zek 2:4-5
[d]**125:3** Es 4:11; Za 89:22; Mit 22:8; Isa 13:11; 14:5; 24:10
[e]**125:4** Za 119:65; 36:10
[f]**125:5** Ay 23:11; Isa 59:8; Za 92:7; 128:6; Mit 2:15; 17:6; Gal 6:16
[g]**126:1** Ezr 1:1-3; Za 85:1; Hos 6:11; Mdo 12:9
[h]**126:2** Mwa 21:6; Ay 8:21; Kum 10:21; Za 65:8; 71:19; Lk 1:49
[i]**126:3** Za 9:2; 16:11; 106:21; Yoe 2:21, 26
[j]**126:4** Kum 30:3; Za 107:35; Isa 43:19; 51:3
[k]**126:5** Za 16:11; 20:5; 23:6; 6:6; 80:5; Yer 50:4; Gal 6:9; Isa 12:1-3; 35:10; 51:11; 60:15; 61:7; Yer 31:6-7, 12
[l]**127:1** Za 78:69; 121:4
[m]**127:2** Mwa 3:17; Hes 6:26; Ay 11:18; Kum 33:12; Mhu 2:25
[n]**127:3** Mwa 1:28; 33:5; Kum 28:4

4 [a]Kama mishale mikononi mwa
shujaa
ndivyo walivyo wana awazaao
mtu katika ujana wake.
5 [b]Heri mtu ambaye podo lake
limejazwa nao.
Hawataaibishwa wanaposhindana
na adui zao langoni.

## Zaburi 128

*Thawabu Ya Kumtii Bwana*

*Wimbo wa kwenda juu.*

1 [c]Heri ni wale wote wamchao Bwana,
waendao katika njia zake.
2 [d]Utakula matunda ya kazi yako;
baraka na mafanikio vitakuwa
vyako.
3 [e]Mke wako atakuwa kama mzabibu
uzaao
ndani ya nyumba yako;
wana wako watakuwa kama
machipukizi ya mizeituni
kuizunguka meza yako.
4 [f]Hivyo ndivyo atakavyobarikiwa
mtu amchaye Bwana.

5 [g]Bwana na akubariki kutoka Sayuni
siku zote za maisha yako,
na uone mafanikio ya Yerusalemu,
6 [h]nawe ujaliwe kuishi uone watoto
wa watoto wako.

Amani iwe juu ya Israeli.

## Zaburi 129

*Maombi Dhidi Ya Adui Za Israeli*

*Wimbo wa kwenda juu.*

1 [i]Wamenionea mno tangu ujana
wangu;
Israeli na aseme sasa:
2 [j]wamenionea mno tangu ujana
wangu,
lakini bado hawajanishinda.
3 [k]Wakulima wamelima mgongo
wangu,
na kufanya mifereji yao mirefu.
4 [l]Lakini Bwana ni mwenye haki;
amenifungua toka kamba za
waovu.

5 [m]Wale wote waichukiao Sayuni
na warudishwe nyuma kwa aibu.
6 [n]Wawe kama majani juu ya paa,
ambayo hunyauka kabla
hayajakua;
7 [o]kwa hayo mvunaji hawezi kujaza
vitanga vyake,
wala akusanyaye kujaza mikono
yake.
8 [p]Wale wapitao karibu na wasiseme,
"Baraka ya Bwana iwe juu yako;
tunakubariki katika jina la
Bwana."

---

[a]**127:4** Za 112:2
[b]**127:5** Za 128:2-3; Mwa 24:60; 23:10
[c]**128:1** Za 103:11; 119:1-3
[d]**128:2** Za 58:11; 109:11; Isa 3:10; Mwa 39:3; Mit 10:22
[e]**128:3** Mwa 49:22; Ay 29:5; Mit 5:15; Eze 19:10; Za 52:8; 144:12
[f]**128:4** Za 1:1; 112:1
[g]**128:5** Za 122:9; 134:3
[h]**128:6** Mwa 50:23; 48:11; Za 125:5
[i]**129:1** Kut 1:13; Eze 23:3; Za 88:15; 124:1; Hos 2:15
[j]**129:2** Yer 1:19; 15:20; 20:11
[k]**129:3** Ebr 11:26
[l]**129:4** Kut 9:27; 2The 1:6; Za 37:9; 140:5
[m]**129:5** Mik 4:11; Za 70:2
[n]**129:6** Isa 37:27; 2Fal 19:26; Za 102:11; 37:2; Yer 17:5-6
[o]**129:7** Kum 28:38; Za 79:12
[p]**129:8** Za 118:26; Rut 2:4

## Zaburi 130

*Kuomba Msaada*

*Wimbo wa kwenda juu.*

1 [a]Kutoka vilindini ninakulilia, Ee
BWANA.
2 [b]Ee BWANA, sikia sauti yangu.
Masikio yako na yawe masikivu
kwa kilio changu unihurumie.

3 [c]Kama wewe, Ee BWANA, ungeweka
kumbukumbu ya dhambi,
Ee Bwana, ni nani angeliweza
kusimama?
4 [d]Lakini kwako kuna msamaha,
kwa hiyo wewe unaogopwa.

5 [e]Namngojea BWANA, nafsi yangu
inangojea,
katika neno lake naweka tumaini
langu.
6 [f]Nafsi yangu inamngojea Bwana
kuliko walinzi waingojeavyo
asubuhi,
naam, kuliko walinzi
waingojeavyo asubuhi.

7 [g]Ee Israeli, mtumaini BWANA,
maana kwa BWANA kuna upendo
usiokoma,
na kwake kuna ukombozi kamili.
8 [h]Yeye mwenyewe ataikomboa Israeli
kutoka dhambi zao zote.

## Zaburi 131

*Kumtegemea Mungu Kwa Unyenyekevu*

*Wimbo wa kwenda juu. Wa Daudi.*

1 [i]Moyo wangu hauna kiburi, Ee
BWANA,
macho yangu hayajivuni;
sijishughulishi na mambo makuu
kunizidi
wala mambo ya ajabu mno
kwangu.
2 [j]Lakini nimetuliza na kunyamazisha
nafsi yangu;
kama mtoto aliyeachishwa
kunyonya na mama yake,
kama mtoto aliyeachishwa kunyonya
ndivyo ilivyo nafsi iliyoko ndani
yangu.

3 [k]Ee Israeli, mtumaini BWANA
tangu sasa na hata milele.

## Zaburi 132

*Maskani Ya Mungu Ya Milele Katika Sayuni*

*Wimbo wa kwenda juu.*

1 Ee BWANA, mkumbuke Daudi
na taabu zote alizozistahimili.

2 [l]Aliapa kiapo kwa BWANA
na akaweka nadhiri kwa Yule
Mwenye Nguvu wa Yakobo:
3 [m]"Sitaingia nyumbani mwangu
au kwenda kitandani mwangu:
4 [n]sitaruhusu usingizi katika macho
yangu,
wala kope zangu kusinzia,
5 [o]mpaka nitakapompatia BWANA
mahali,
makao kwa ajili ya Yule Mwenye
Nguvu wa Yakobo."

---

[a]**130:1** Ay 30:19
[b]**130:2** Za 27:7; 28:2, 6; 31:22; 86:6; 140:6; 2Nya 6:40
[c]**130:3** 1Sam 6:20; Ezr 9:15; Hes 1:6; Za 143:2; Ufu 6:17; Yn 8:7, 9; Rum 3:20
[d]**130:4** Kut 34:7; Efe 1:7; 2Sam 24:14; Yer 17:5-6; 31:34; 1Fal 8:40; 2The 1:6; Za 37:2; Ebr 12:28
[e]**130:5** Isa 8:17; 26:8; 30:18; 49:23; Za 5:3; 119:74; 27:14
[f]**130:6** Za 63:6; 2Sam 23:4
[g]**130:7** 1Nya 21:13; Za 25:5; 71:14; 111:9; Rum 3:24; Isa 55:7
[h]**130:8** Lk 1:68; Kut 34:7; Mt 1:21
[i]**131:1** Isa 2:12; Yer 45:5; Rum 12:16; 2Sam 22:28; Ay 41:34; 5:9; Za 101:5; 139:6
[j]**131:2** Za 116:7; Mit 18:3; Mt 18:3; 1Kor 13:11; 14:20
[k]**131:3** Za 25:5; 130:7; 113:2; 119:43
[l]**132:2** Mwa 49:24; Isa 49:26; 60:16
[m]**132:3** 2Sam 7:2, 27
[n]**132:4** Rut 3:18
[o]**132:5** 1Fal 8:17; Mdo 7:46

6 [a]Tulisikia habari hii huko Efrathi,
tulikutana nayo katika mashamba
ya Yaara:[b]
7 [c]"Twendeni kwenye makao yake,
na tuabudu kwenye kiti cha
kuwekea miguu yake;
8 [d]inuka, Ee BWANA, uje mahali pako
pa kupumzikia,
wewe na Sanduku la nguvu zako.
9 [e]Makuhani wako na wavikwe haki,
watakatifu wako na waimbe kwa
furaha."

10 Kwa ajili ya Daudi mtumishi wako,
usimkatae mpakwa mafuta wako.

11 [f]BWANA alimwapia Daudi kiapo,
kiapo cha uhakika ambacho
hatakitangua:
"Nitamweka mmoja wa wazao wako
mwenyewe
katika kiti chako cha enzi,
12 [g]kama wanao watashika Agano langu
na sheria ninazowafundisha,
ndipo wana wao watarithi
kiti chako cha enzi milele na
milele."

13 [h]Kwa maana BWANA ameichagua
Sayuni,
amepaonea shauku pawe maskani
yake:
14 [i]"Hapa ni mahali pangu pa
kupumzika milele na milele;
hapa ndipo nitakapoketi
nikitawala, kwa sababu
nimepaonea shauku:
15 [j]Nitambariki kwa kumpa mahitaji
tele:
nitashibisha maskini wake kwa
chakula.
16 [k]Nitawavika makuhani wake
wokovu,
nao watakatifu wake watadumu
wakiimba kwa furaha.

17 [l]"Hapa nitamchipushia Daudi
pembe,[m]
na kuweka taa kwa ajili ya masiya[n]
wangu.
18 [o]Adui zake nitawavika aibu,
bali taji kichwani pake itang'aa
sana."

## Zaburi 133

*Sifa Za Pendo La Undugu*

*Wimbo wa kwenda juu. Wa Daudi.*

1 [p]Tazama jinsi ilivyo vyema na
kupendeza
wakati ndugu wanapoishi pamoja
katika umoja!
2 [q]Ni kama mafuta ya thamani
yaliyomiminwa kichwani,
yakitiririka kwenye ndevu,
yakitiririka kwenye ndevu za Aroni,
mpaka kwenye upindo wa mavazi
yake.
3 [r]Ni kama vile umande wa Hermoni
unavyoanguka juu ya Mlima
Sayuni.
Kwa maana huko ndiko BWANA
alikoamuru baraka yake,
naam, hata uzima milele.

---

[a]**132:6** 1Sam 7:2; 17:12; Yos 9:17; 18:1; 1Nya 13:5
[b]6 Yaani Kiriath-Yearimu.
[c]**132:7** 2Sam 15:25; Za 5:7; 122:1; 1Nya 28:2
[d]**132:8** Hes 10:35
[e]**132:9** Ay 27:6; Zek 3:4; Isa 61:3, 10; Mal 3:3; Ay 29:14
[f]**132:11** Za 89:3-4, 35; 1Nya 17:11-14; Mt 1:1; Lk 3:31
[g]**132:12** 2Nya 6:16; Za 25:10; Lk 1:32; Mdo 2:30
[h]**132:13** Kut 15:17; Za 48:1, 2; 68:16; 1Fal 18:13
[i]**132:14** Za 80:1; 68:16; 2Sam 6:2
[j]**132:15** Za 107:9; 147:14
[k]**132:16** 2Nya 6:41; Ay 8:21; Za 149:5
[l]**132:17** 1Sam 2:10; Za 18:28; 84:9; 92:10; Eze 29:21; Lk 1:69; 1Fal 11:36; 2Fal 8:19; 2Nya 21:7
[m]17 Pembe inawakilisha nguvu.
[n]17 Masiya yaani mpakwa mafuta.
[o]**132:18** Ay 8:22; 2Sam 12:30
[p]**133:1** Mwa 13:8; Yn 17:11; 1Kor 1:10; Rum 12:10
[q]**133:2** Kut 29:7; 30:25
[r]**133:3** Ay 29:19; Mit 19:12; Isa 18:4; 26:19; 45:8; Hos 14:5; Mik 5:7; Kum 3:8; Kut 15:17; Law 25:21; Za 2:6; 74:2; 21:4; Dan 12:2-3; Yn 4:14; Ebr 7:25; 1Yn 5:20

## Zaburi 134

*Wito Wa Kumsifu Mungu*

*Wimbo wa kwenda juu.*

1 [a]Msifuni BWANA, ninyi nyote
watumishi wa BWANA,
ninyi mnaotumika usiku ndani ya
nyumba ya BWANA.
2 [b]Inueni mikono yenu katika pale
patakatifu
na kumsifu BWANA.

3 [c]Naye BWANA, Muumba wa mbingu
na dunia,
awabariki kutoka Sayuni.

## Zaburi 135

*Wimbo Wa Sifa Kwa Mungu*

1 [d]Msifuni BWANA.

Lisifuni jina la BWANA,
msifuni, enyi watumishi wa
BWANA,
2 [e]ninyi ambao mnatumika ndani ya
nyumba ya BWANA,
katika nyua za nyumba ya Mungu
wetu.

3 [f]Msifuni BWANA, kwa kuwa BWANA
ni mwema,
liimbieni sifa jina lake, kwa maana
hilo lapendeza.
4 [g]Kwa maana BWANA amemchagua
Yakobo kuwa wake
mwenyewe,
Israeli kuwa mali yake ya
thamani.

5 [h]Ninajua ya kuwa BWANA ni mkuu,
kwamba Bwana wetu ni mkuu
kuliko miungu yote.
6 [i]BWANA hufanya lolote apendalo,
mbinguni na duniani,
katika bahari na vilindi vyake
vyote.
7 [j]Hufanya mawingu kupanda kutoka
miisho ya dunia;
hupeleka umeme wa radi pamoja
na mvua
na huleta upepo kutoka ghala
zake.

8 [k]Alimuua mzaliwa wa kwanza wa
Misri,
mzaliwa wa kwanza wa
wanadamu na wanyama.
9 [l]Alipeleka ishara zake na maajabu
katikati yako, ee Misri,
dhidi ya Farao na watumishi wake
wote.
10 [m]Aliyapiga mataifa mengi,
na akaua wafalme wenye nguvu:
11 [n]Mfalme Sihoni na Waamori,
Ogu mfalme wa Bashani
na wafalme wote wa Kanaani:
12 [o]akatoa nchi yao kuwa urithi,
urithi kwa watu wake Israeli.

13 [p]Ee BWANA, jina lako ladumu milele,
kumbukumbu za fahari zako, Ee
BWANA, kwa vizazi vyote.
14 [q]Maana BWANA atawathibitisha watu
wake,
na kuwahurumia watumishi wake.

15 [r]Sanamu za mataifa ni fedha na
dhahabu,
zilizotengenezwa kwa mikono ya
wanadamu.

---

[a]**134:1** Za 130:6; 113:1; 135:1, 2; Ufu 19:5; Lk 2:37; 1Nya 15:2; 23:30; Hes 16:9
[b]**134:2** Za 33:2; 103:1; 28:2; 1Tim 2:8
[c]**134:3** Za 124:8; 20:2; 128:5; Law 25:21
[d]**135:1** Neh 7:73
[e]**135:2** 1Nya 15:2; Lk 2:37; Za 116:19
[f]**135:3** 1Nya 16:34; Za 119:68; 68:4; 92:1; 147:1
[g]**135:4** Kut 19:5; Kum 7:6, 7; 10:15; Mal 3:17; Tit 2:14
[h]**135:5** Za 48:1; 145:3; Kut 12:12; 1Nya 16:25; Ay 21:22
[i]**135:6** Za 115:3; Dan 4:35; Mt 6:10
[j]**135:7** Ay 5:10; Za 68:6; Isa 30:23; Amo 4:13; Yer 10:13; 51:16; Yoe 2:23; Zek 10:1; Kum 28:12; Mwa 2:6; Ay 28:25; 38:22
[k]**135:8** Kut 4:23; 12:12
[l]**135:9** Kut 7:9; Za 136:10-15
[m]**135:10** Hes 21:21-25; Yos 24:8-11; Za 44:2; 78:55; 136:17-21
[n]**135:11** Hes 21:21, 26, 33; Yos 12:7-24
[o]**135:12** Kum 29:8
[p]**135:13** Kut 3:15; Za 102:12
[q]**135:14** 1Sam 24:15; Ebr 10:30; Kum 32:36
[r]**135:15** Ufu 9:20; Isa 2:8; 31:7; 37:19; 40:19; Yer 1:16; 10:5; Za 96:5

16 [a]Zina vinywa, lakini haziwezi
kusema,
zina macho, lakini haziwezi
kuona;
17 [b]zina masikio, lakini haziwezi
kusikia,
wala hakuna pumzi katika vinywa
vyao.
18 Wale wanaozitengeneza watafanana
nazo,
vivyo hivyo wale wote
wanaozitumainia.

19 [c]Ee nyumba ya Israeli, msifuni
Bwana;
ee nyumba ya Aroni, msifuni
Bwana;
20 ee nyumba ya Lawi, msifuni Bwana;
ninyi mnaomcha, msifuni Bwana.
21 [d]Msifuni Bwana kutoka Sayuni,
msifuni yeye aishiye Yerusalemu.

Msifuni Bwana.

## Zaburi 136

*Wimbo Wa Kumshukuru Mungu*

1 [e]Mshukuruni Bwana, kwa kuwa ni
mwema.
*Fadhili zake zadumu milele.*
2 [f]Mshukuruni Mungu wa miungu.
*Fadhili zake zadumu milele.*
3 [g]Mshukuruni Bwana wa mabwana:
*Fadhili zake zadumu milele.*

4 [h]Kwake yeye pekee atendaye
maajabu makuu,
*Fadhili zake zadumu milele.*
5 [i]Ambaye kwa ufahamu wake
aliziumba mbingu,
*Fadhili zake zadumu milele.*
6 [j]Ambaye aliitandaza dunia juu ya
maji,
*Fadhili zake zadumu milele.*
7 [k]Ambaye aliumba mianga mikubwa,
*Fadhili zake zadumu milele.*
8 [l]Jua litawale mchana,
*Fadhili zake zadumu milele.*
9 Mwezi na nyota vitawale usiku,
*Fadhili zake zadumu milele.*

10 [m]Kwake yeye aliyemuua mzaliwa wa
kwanza wa Misri,
*Fadhili zake zadumu milele.*
11 [n]Na kuwatoa Israeli katikati yao,
*Fadhili zake zadumu milele.*
12 [o]Kwa mkono wenye nguvu
ulionyooshwa,
*Fadhili zake zadumu milele.*

13 [p]Kwake yeye aliyeigawa Bahari ya
Shamu,
*Fadhili zake zadumu milele.*
14 [q]Na kuwapitisha Israeli katikati yake,
*Fadhili zake zadumu milele.*
15 [r]Lakini alimfagia Farao na jeshi lake
katika Bahari ya Shamu,
*Fadhili zake zadumu milele.*

16 [s]Kwake yeye aliyewaongoza watu
wake katika jangwa,
*Fadhili zake zadumu milele.*
17 [t]Ambaye aliwapiga wafalme wenye
nguvu,
*Fadhili zake zadumu milele.*
18 [u]Naye aliwaua wafalme wenye
nguvu,
*Fadhili zake zadumu milele.*

---

[a]**135:16** 1Fal 18:26
[b]**135:17** Yer 10:14; Hab 2:19
[c]**135:19** Za 22:23
[d]**135:21** Za 128:5; 134:3; 1Fal 8:13; 2Nya 6:2
[e]**136:1** Za 105:1; 100:5; 145:9; 118:1-4; 106:1; Ezr 3:11; Hes 2:26; 1:7; 2Nya 5:13; Yer 33:11
[f]**136:2** Za 105:1; Kum 10:17; Kut 18:11
[g]**136:3** Za 105:1; Kum 10:17; 1Tim 6:15
[h]**136:4** Kut 3:20; Ay 9:10
[i]**136:5** Mit 3:19; Yer 51:15; Mwa 1:1
[j]**136:6** Mwa 1:1; 1:6; Isa 42:5; Yer 10:12; 33:2
[k]**136:7** Mwa 1:14, 16; Za 74:16; Yak 1:17
[l]**136:8** Mwa 1:16
[m]**136:10** Kut 4:23; 12:12
[n]**136:11** Kut 6:6; 13:3; Za 105:43
[o]**136:12** Kut 3:20; Kum 5:15; 9:29
[p]**136:13** Za 78:13
[q]**136:14** Kut 14:22; Za 106:9
[r]**136:15** Kut 14:27
[s]**136:16** Kut 13:18; Za 78:52
[t]**136:17** Hes 21:23-25; Yos 24:8-11; Za 78:55; 135:9-12
[u]**136:18** Kum 29:7; Yos 12:7-24

19 [a]Sihoni mfalme wa Waamori,
*Fadhili zake zadumu milele.*
20 [b]Ogu mfalme wa Bashani,
*Fadhili zake zadumu milele.*
21 [c]Akatoa nchi yao kuwa urithi,
*Fadhili zake zadumu milele.*
22 [d]Urithi kwa Israeli mtumishi wake,
*Fadhili zake zadumu milele.*

23 [e]Aliyetukumbuka katika unyonge wetu,
*Fadhili zake zadumu milele.*
24 [f]Alituweka huru toka adui zetu,
*Fadhili zake zadumu milele.*
25 [g]Ambaye humpa chakula kila kiumbe.
*Fadhili zake zadumu milele.*

26 [h]Mshukuruni Mungu wa mbinguni,
*Fadhili zake zadumu milele.*

## Zaburi 137

*Maombolezo Ya Israeli Uhamishoni*

1 [i]Kando ya mito ya Babeli tuliketi, tukaomboleza
tulipokumbuka Sayuni.
2 [j]Kwenye miti ya huko
tulitundika vinubi vyetu,
3 [k]kwa maana huko hao waliotuteka
walitaka tuwaimbie nyimbo,
watesi wetu walidai nyimbo za furaha;
walisema, "Tuimbieni wimbo mmoja kati ya nyimbo za Sayuni!"
4 [l]Tutaimbaje nyimbo za BWANA,
tukiwa nchi ya kigeni?
5 [m]Nikikusahau wewe, ee Yerusalemu,
basi mkono wangu wa kuume na usahau ujuzi wake.
6 [n]Ulimi wangu ushikamane na kaakaa la kinywa changu
kama sitakukumbuka wewe,
kama nisipokufikiri Yerusalemu
kuwa furaha yangu kubwa.

7 [o]Kumbuka, Ee BWANA, walichokifanya Waedomu,
siku ile Yerusalemu ilipoanguka.
Walisema, "Bomoa, Bomoa
mpaka kwenye misingi yake!"

8 [p]Ee binti Babeli, uliyehukumiwa kuangamizwa,
heri yeye atakayekulipiza wewe
kwa yale uliyotutenda sisi:
9 [q]yeye ambaye atawakamata watoto wako wachanga
na kuwaponda juu ya miamba.

## Zaburi 138

*Maombi Ya Shukrani*

*Zaburi ya Daudi.*

1 [r]Nitakusifu wewe, Ee BWANA, kwa moyo wangu wote,
mbele ya "miungu" nitaimba sifa zako.
2 [s]Nitasujudu nikielekea Hekalu lako takatifu,
nami nitalisifu jina lako
kwa ajili ya upendo wako
na uaminifu,

---

[a]**136:19** Hes 21:21-25
[b]**136:20** Hes 21:33-35
[c]**136:21** Kum 1:38; Yos 12:1; 14:1
[d]**136:22** Kum 29:8; Za 78:55; Isa 20:3; 41:8; 42:19; 43:10; 44:1, 21; 45:4; 49:5-7
[e]**136:23** Za 78:29; 103:14; 115:12
[f]**136:24** Yos 10:14; Neh 9:28; Kum 6:19
[g]**136:25** Mwa 1:30; Mit 6:26
[h]**136:26** Za 105:1; 115:3; Ezr 3:11
[i]**137:1** Eze 1:1; Dan 8:2
[j]**137:2** Isa 24:8; Ay 30:9; 30:31; Ufu 18:22; Amo 6:5; 8:10; Mao 1:5; 5:15; Za 79:1-4; 80:6; Eze 16:57; 22:4; 34:29; 26:13
[k]**137:3** Mao 1:5; Za 79:1-4; 80:6; Eze 16:57; 22:4; 34:29; Ay 30:9
[l]**137:4** Neh 12:46
[m]**137:5** Isa 2:3; 56:7; 65:11; 66:20
[n]**137:6** Za 22:15; Neh 2:3; Yer 51:50; Kum 4:29; Eze 3:26; 6:9
[o]**137:7** Mwa 25:30; 2Nya 28:17; Za 74:8; 83:6; Mao 1:10; 4:21-22; 2Fal 25:1-10
[p]**137:8** Yer 25:12, 26; 50:1; Isa 13:1, 19; 47:1-15
[q]**137:9** 2Fal 8:12; Isa 13:16; Lk 19:44
[r]**138:1** Za 95:3; 96:4; 27:6; 108:1
[s]**138:2** 1Fal 8:29; Za 74:21; 97:12; 5:7; 108:4; 115:1; 140:13; 119:9

kwa kuwa umelikuza jina lako na neno lako
juu ya vitu vyote.
3 [a]Nilipoita, ulinijibu;
ulinifanya jasiri na mwenye moyo hodari.

4 [b]Wafalme wote wa dunia wakusifu wewe Ee BWANA,
wakati wanaposikia maneno ya kinywa chako.
5 [c]Wao na waimbe kuhusu njia za BWANA,
kwa maana utukufu wa BWANA ni mkuu.

6 [d]Ingawa BWANA yuko juu,
humwangalia mnyonge,
bali mwenye kiburi
yeye anamjua kutokea mbali.
7 [e]Nijapopita katikati ya shida,
wewe unayahifadhi maisha yangu,
unanyoosha mkono wako dhidi ya hasira ya adui zangu,
kwa mkono wako wa kuume unaniokoa.
8 [f]BWANA atatimiza kusudi lake kwangu,
Ee BWANA, upendo wako wadumu milele:
usiziache kazi za mikono yako.

## Zaburi 139

*Mungu Asiyeweza Kukwepwa*

*Kwa mwimbishaji. Zaburi ya Daudi.*

1 [g]Ee BWANA, umenichunguza
na kunijua.
2 [h]Unajua ninapoketi na ninapoinuka;
unatambua mawazo yangu tokea mbali.
3 [i]Unafahamu kutoka kwangu na kulala kwangu;
unaelewa njia zangu zote.
4 [j]Kabla neno halijafika katika ulimi wangu,
wewe walijua kikamilifu, Ee BWANA.

5 [k]Umenizunguka nyuma na mbele;
umeweka mkono wako juu yangu.
6 [l]Maarifa haya ni ya ajabu mno kwangu,
ni ya juu sana kwangu kuyafikia.

7 [m]Niende wapi nijiepushe na Roho yako?
Niende wapi niukimbie uso wako?
8 [n]Kama nikienda juu mbinguni, wewe uko huko;
nikifanya vilindi[o] kuwa kitanda changu,
wewe uko huko.
9 Kama nikipanda juu ya mbawa za mapambazuko,
kama nikikaa pande za mbali za bahari,
10 [p]hata huko mkono wako utaniongoza,
mkono wako wa kuume utanishika kwa uthabiti.

11 Kama nikisema, "Hakika giza litanificha
na nuru inayonizunguka iwe usiku,"

[a]**138:3** Za 28:7; 18:6; 30:2; 99:6; 116:4; 118:5; Mit 28:1; Mdo 4:29
[b]**138:4** Za 72:11; 102:15
[c]**138:5** Za 51:14; 71:16; 145:7; 21:5
[d]**138:6** Za 113:6; 40:4; Mt 23:12
[e]**138:7** Za 7:6; 23:4; 41:2; 20:6; 60:5; 108:6; 17:7, 14; Kut 7:5
[f]**138:8** Flp 1:6; Ezr 3:11; Za 100:5; 51:11; Ay 10:3, 8
[g]**139:1** Za 17:3; 44:21; Rum 8:27
[h]**139:2** 2Fal 19:27; Za 94:11; Mit 24:12; Yer 12:3
[i]**139:3** 2Fal 19:27; Ay 31:4
[j]**139:4** Ebr 4:13
[k]**139:5** 1Sam 25:16; Za 32:10; 34:7; 125:2
[l]**139:6** Za 131:1; Rum 11:33
[m]**139:7** Yer 23:24
[n]**139:8** Kum 30:12-15; Amo 9:2-3; Ay 17:13
[o]8 Vilindi ina maana ya Kuzimu, ambayo ni Sheol kwa Kiebrania.
[p]**139:10** Za 23:3; 108:6; Isa 41:10

12 [a]hata giza halitakuwa giza kwako,
usiku utang'aa kama mchana,
kwa kuwa giza ni kama nuru
kwako.

13 [b]Kwa maana wewe ndiwe uliyeumba
utu wangu wa ndani;
uliniunga pamoja tumboni mwa
mama yangu.
14 Ninakusifu kwa sababu nimeumbwa
kwa namna ya ajabu na ya
kutisha;
kazi zako ni za ajabu,
ninajua hayo kikamilifu.
15 [c]Umbile langu halikufichika kwako,
nilipoumbwa mahali pa siri.
Nilipoungwa pamoja kwa ustadi
katika vilindi vya nchi,
16 [d]macho yako yaliniona kabla
mwili wangu haujakamilika.
Siku zangu zote ulizonipangia
ziliandikwa katika kitabu chako
kabla haijakuwepo hata moja.

17 [e]Tazama jinsi yalivyo ya thamani
mawazo yako kwangu, Ee
Mungu!
Jinsi jumla yake ilivyo kubwa!
18 [f]Kama ningezihesabu,
zingekuwa nyingi kuliko mchanga.
Niamkapo,
bado niko pamoja nawe.

19 [g]Laiti ungewachinja waovu, Ee
Mungu!
Ondokeni kwangu, ninyi
wamwaga damu!
20 [h]Wanazungumza juu yako wakiwa na
kusudi baya,
adui zako wanatumia vibaya jina
lako.
21 [i]Ee BWANA, je, nisiwachukie
wanaokuchukia?
Nisiwachukie sana wanaoinuka
dhidi yako?
22 [j]Sina kitu zaidi ya chuki dhidi yao,
ninawahesabu ni adui zangu.

23 [k]Ee Mungu, nichunguze, uujue moyo
wangu,
nijaribu na ujue mawazo yangu.
24 [l]Uone kama kuna njia iletayo
machukizo ndani yangu,
uniongoze katika njia ya milele.

## Zaburi 140

*Kuomba Ulinzi Wa Mungu*

*Kwa mwimbishaji. Zaburi ya Daudi.*

1 [m]Ee BWANA, niokoe, kutoka kwa
watu waovu;
nilinde na watu wenye jeuri,
2 [n]ambao hupanga mipango mibaya
mioyoni mwao,
na kuchochea vita siku zote.
3 [o]Wao hufanya ndimi zao kali kama
za nyoka,
sumu ya nyoka iko midomoni
mwao.

4 [p]Ee BWANA, niepushe na mikono ya
waovu;
nilinde na watu wenye jeuri
wanaopanga kunikwaza miguu
yangu.

---

[a]**139:12** Ay 34:22; Dan 2:22
[b]**139:13** Za 119:73; Ay 10:11; Isa 44:2, 24; 46:3; 49:5; Yer 1:5
[c]**139:15** Mhu 11:5; Ay 10:11; Za 63:9
[d]**139:16** Ay 33:29; Za 90:12
[e]**139:17** Za 92:5; Ay 5:9
[f]**139:18** Za 40:5; 3:5; Ay 29:18
[g]**139:19** Za 5:6; 6:8; 59:2; Isa 11:4
[h]**139:20** Za 65:7; Kum 5:11; Ay 21:14-15; Yud 15
[i]**139:21** 2Nya 19:2; Za 31:6; 26:5; 119:113
[j]**139:22** Mt 5:43
[k]**139:23** Ay 31:6; 1Sam 16:7; 1Nya 29:17; Za 7:9; Mit 17:3; Yer 11:20; Ufu 2:23
[l]**139:24** Yer 25:5; 36:3; Za 5:8; 23:2; 143:10
[m]**140:1** Za 17:13; 25:20; 59:2; 71:4; 142:6; 143:9; 86:14
[n]**140:2** Mit 6:14; 16:27; Isa 59:4; Hos 7:15; Za 36:4; 52:2; 68:30
[o]**140:3** Za 57:4; 58:4; Rum 3:13; Yak 3:8
[p]**140:4** Za 141:9; 36:11

[5] [a]Wenye kiburi wameficha mtego wa kuninasa,
wametandaza kamba za wavu wao,
wametega mitego kwenye njia yangu.

[6] [b]Ee BWANA, ninakuambia, "Wewe ni Mungu wangu."
Ee BWANA, usikie kilio changu na kunihurumia.
[7] Ee BWANA Mwenyezi, Mwokozi wangu mwenye nguvu,
unikingaye kichwa changu siku ya vita:
[8] [c]Ee BWANA, usiwape waovu matakwa yao,
usiache mipango yao ikafanikiwa,
wasije wakajisifu.

[9] [d]Vichwa vya wanaonizunguka vifunikwe
na shida zinazosababishwa na midomo yao.
[10] [e]Makaa ya mawe ya moto na yawaangukie!
Na watupwe motoni,
katika mashimo ya matope,
wasiinuke tena kamwe.
[11] [f]Wasingiziaji wasifanikiwe katika nchi;
maafa na yawawinde watu wenye jeuri.

[12] [g]Najua kwamba BWANA huwapatia maskini haki,
na kuitegemeza njia ya mhitaji.
[13] [h]Hakika wenye haki watalisifu jina lako,
na waadilifu wataishi mbele zako.

## Zaburi 141

*Maombi Ya Kuhifadhiwa Dhidi Ya Uovu*

*Zaburi ya Daudi.*

[1] [i]Ee BWANA, ninakuita wewe, uje kwangu hima.
Sikia sauti yangu ninapokuita.
[2] [j]Maombi yangu na yafike mbele zako kama uvumba;
kuinua mikono yangu juu na kuwe kama dhabihu ya jioni.

[3] [k]Ee BWANA, weka mlinzi kinywani mwangu,
weka ulinzi mlangoni mwa midomo yangu.
[4] [l]Usiuache moyo wangu uvutwe katika jambo baya,
nisije nikashiriki katika matendo maovu
pamoja na watu watendao mabaya,
wala nisije nikala vyakula vyao vya anasa.

[5] [m]Mtu mwenye haki na anipige: ni jambo la huruma;
na anikemee: ni mafuta kichwani mwangu.
Kichwa changu hakitalikataa.

Hata hivyo, maombi yangu daima
ni kinyume cha watenda mabaya,
[6] [n]watawala wao watatupwa chini
kutoka kwenye majabali,
waovu watajifunza kwamba maneno yangu
yalikuwa kweli.
[7] [o]Watasema, "Kama mtu anavyolima na kuvunja ardhi,
ndivyo mifupa yetu imetawanywa kwenye mlango wa kaburi."

---

[a]**140:5** Ay 34:30; Za 31:4; 38:12; 119:110; Ay 18:8; 18:9
[b]**140:6** Za 16:2; 28:2, 6
[c]**140:8** Za 10:2-3; 66:7; Ay 5:12-13
[d]**140:9** Mit 18:7
[e]**140:10** Za 11:6; 21:9; Mt 3:10; Lk 12:40; Ufu 20:15
[f]**140:11** Za 34:21
[g]**140:12** 1Fal 8:45; Za 35:10; 82:3; 109:31
[h]**140:13** Za 138:2; 11:7; 16:11
[i]**141:1** Za 22:19; 4:1; 5:1-2; 27:7; 143:1
[j]**141:2** Lk 1:9; Ufu 5:8; 8:3; Za 28:2; 63:4; 1Tim 2:8; Kut 29:39, 41; 30:8; Efe 5:2
[k]**141:3** Za 34:13; 12:2; Yak 1:26; 3:8
[l]**141:4** Yos 24:23; Za 106:29; Mit 23:1-3
[m]**141:5** Mit 9:8; 19:25; 25:12; Mhu 7:5; Kut 29:7; Za 23:5
[n]**141:6** 2Nya 25:12
[o]**141:7** Za 129:3; Hes 16:32-33; 16:30; 2Kor 1:9

8 [a]Lakini nimekaza macho yangu
kwako, Ee BWANA Mwenyezi,
ndani yako nimekimbilia,
usiniache nife.
9 [b]Niepushe na mitego waliyonitegea,
kutokana na mitego iliyotegwa na
watenda mabaya.
10 [c]Waovu na waanguke kwenye nyavu
zao wenyewe,
wakati mimi ninapita salama.

## Zaburi 142

*Maombi Ya Kuokolewa Dhidi Ya Watesi*

*Utenzi wa Daudi. Alipokuwa pangoni. Maombi.*

1 [d]Namlilia BWANA kwa sauti,
nainua sauti yangu kwa BWANA
anihurumie.
2 [e]Namimina malalamiko yangu mbele
zake,
mbele zake naeleza shida zangu.

3 [f]Wakati roho yangu inapozimia
ndani yangu,
wewe ndiwe unajua njia zangu.
Katika njia ninayopita
watu wameniwekea mtego.
4 [g]Tazama kuume kwangu na uone,
hakuna hata mmoja
anayejihusisha nami.
Sina kimbilio,
hakuna anayejali maisha yangu.

5 [h]Ee BWANA, nakulilia wewe,
nasema, "Wewe ni kimbilio langu,
fungu langu katika nchi ya walio
hai."
6 [i]Sikiliza kilio changu,
kwa sababu mimi ni mhitaji sana;
niokoe na wale wanaonifuatilia,
kwa kuwa wamenizidi nguvu.
7 [j]Nifungue kutoka kifungo changu,
ili niweze kulisifu jina lako.

Ndipo wenye haki watanizunguka,
kwa sababu ya wema wako
kwangu.

## Zaburi 143

*Maombi Ya Kuokolewa Dhidi Ya Adui*

*Zaburi ya Daudi.*

1 [k]Ee BWANA, sikia sala yangu,
sikiliza kilio changu unihurumie;
katika uaminifu na haki yako
njoo unisaidie.
2 [l]Usimhukumu mtumishi wako,
kwa kuwa hakuna mtu anayeishi
aliye mwenye haki mbele
zako.

3 [m]Adui hunifuatilia,
hunipondaponda chini;
hunifanya niishi gizani
kama wale waliokufa zamani.
4 [n]Kwa hiyo roho yangu inazimia
ndani yangu,
moyo wangu ndani yangu unakata
tamaa.

5 [o]Nakumbuka siku za zamani;
natafakari juu ya kazi zako zote,
naangalia juu ya kazi
ambazo mikono yako imezifanya.
6 [p]Nanyoosha mikono yangu kwako,
nafsi yangu inakuonea kiu kama
ardhi kame.

7 [q]Ee BWANA, unijibu haraka,
roho yangu inazimia.
Usinifiche uso wako,
ama sivyo nitafanana na wale
washukao shimoni.

---

[a]**141:8** Za 123:2; 2:12; 11:1
[b]**141:9** Za 140:4; 64:5; 38:12
[c]**141:10** Za 7:15; 35:8; 57:6; 124:7
[d]**142:1** 1Fal 8:52; Za 3:4; 30:8
[e]**142:2** Za 64:1; 50:15
[f]**142:3** Za 6:2; 77:3; 84:2; 88:4; 143:4, 7; Yer 4:18; Mao 1:22
[g]**142:4** Yer 25:35; 30:17
[h]**142:5** Za 16:5; 27:13; 46:1; Kum 32:9; Ay 28:13; Mao 3:24
[i]**142:6** Za 17:1; 79:8; 25:20; Yer 31:11
[j]**142:7** Za 66:11; 7:17; 9:2; 2Nya 6:41
[k]**143:1** Za 141:1; 28:2; 130:2; 89:1-2
[l]**143:2** Za 14:3; Rum 3:10; Ay 14:3; 4:17; Mhu 7:20; Gal 2:16
[m]**143:3** Za 107:10; 7:1, 2; Law 3:6
[n]**143:4** Za 30:7
[o]**143:5** Za 77:6; 77:5, 11; Mwa 24:63
[p]**143:6** Kut 9:29; Ay 11:13; Za 28:2
[q]**143:7** Za 69:17; 142:3; 22:24; 27:9; 30:7

8 [a]Asubuhi uniletee neno la upendo
wako usiokoma,
kwa kuwa nimeweka tumaini
langu kwako.
Nionyeshe njia nitakayoiendea,
kwa kuwa kwako nainua nafsi
yangu.
9 [b]Ee BWANA, uniokoe na adui zangu,
kwa kuwa nimejificha kwako.
10 [c]Nifundishe kufanya mapenzi yako,
kwa maana wewe ndiwe Mungu
wangu,
Roho wako mwema na aniongoze
katika nchi tambarare.

11 [d]Ee BWANA, kwa ajili ya jina lako,
hifadhi maisha yangu,
kwa haki yako nitoe katika taabu.
12 [e]Kwa upendo wako usiokoma,
nyamazisha adui zangu;
waangamize watesi wangu wote,
kwa kuwa mimi ni mtumishi
wako.

## Zaburi 144

*Mfalme Amshukuru Mungu Kwa Ushindi*

*Zaburi ya Daudi.*

1 [f]Sifa ni kwa BWANA Mwamba
wangu,
aifundishaye mikono yangu vita,
na vidole vyangu kupigana.
2 [g]Yeye ni Mungu wangu wa upendo
na boma langu,
ngome yangu na mwokozi wangu,
ngao yangu ninayemkimbilia,
ambaye huwatiisha mataifa chini
yangu.
3 [h]Ee BWANA, mwanadamu ni nini
hata umjali,
Binadamu ni nini hata umfikirie?
4 [i]Mwanadamu ni kama pumzi,
siku zake ni kama kivuli
kinachopita.

5 [j]Ee BWANA, pasua mbingu zako,
ushuke,
gusa milima ili itoe moshi.
6 [k]Peleka umeme uwatawanye adui,
lenga mishale yako uwashinde.
7 [l]Nyoosha mkono wako kutoka juu,
nikomboe na kuniokoa
kutoka maji makuu,
kutoka mikononi mwa wageni
8 [m]ambao vinywa vyao vimejaa uongo,
na mikono yao ya kuume ni
midanganyifu.

9 [n]Ee Mungu, nitakuimbia wimbo
mpya,
kwa zeze yenye nyuzi kumi
nitakuimbia,
10 [o]kwa Yule awapaye wafalme ushindi,
ambaye humwokoa Daudi,
mtumishi wake kutokana na
upanga hatari.

11 [p]Nikomboe na uniokoe
kutoka mikononi mwa wageni
ambao vinywa vyao vimejaa uongo,
na mikono yao ya kuume ni
midanganyifu.

---

[a]**143:8** Kut 33:13; Ay 34:32; Za 6:4; 90:14; 27:11; 32:8; 25:1-2; 86:4
[b]**143:9** Za 140:1; 18:17; 31:15
[c]**143:10** Za 119:12; 31:14; 25:4-5; 26:11; Neh 9:20; Yn 14:26; Rum 5:5; Efe 4:30; Gal 5:22, 23
[d]**143:11** Za 25:11; 41:2; 31:1; 71:2
[e]**143:12** Za 8:2; 54:5; 116:16
[f]**144:1** Mwa 49:24; 2Sam 22:35
[g]**144:2** Za 59:9; 91:2; 18:39; 27:1; 37:39; 43:2; 18:2; Amu 4:23; Mwa 15:1
[h]**144:3** Ebr 2:6
[i]**144:4** Ay 7:7; 27:3; 14:2; Isa 2:22; 1Nya 29:15; Yak 4:14
[j]**144:5** Za 18:9; 57:3; 104:32; Isa 64:1; Mwa 11:5
[k]**144:6** Hab 3:11; Zek 9:14; Za 59:11; 68:1; 7:12, 13; 18:14
[l]**144:7** 2Sam 22:17; Za 3:7; 57:3; 69:2; 18:44
[m]**144:8** Za 12:2; 41:6; 26:3; Mwa 14:22; Kum 32:40
[n]**144:9** Za 28:7; 96:1; 33:2-3; 71:22; 69:1
[o]**144:10** 2Sam 8:14; Za 18:50; Ay 5:20
[p]**144:11** Za 3:7; 25:20; 18:44; 41:6-7; 12:2; 36:3; 106:26; Isa 44:20

12 [a]Kisha wana wetu wakati wa ujana
wao
watakuwa kama mimea
iliyotunzwa vizuri,
binti zetu watakuwa kama nguzo
zilizoviringwa
kurembesha jumba la kifalme.
13 [b]Ghala zetu zitajazwa
aina zote za mahitaji.
Kondoo zetu watazaa kwa maelfu,
kwa makumi ya maelfu katika
mashamba yetu;
14 [c]maksai wetu watakokota
mizigo mizito.
Hakutakuwa na kubomoka kuta,
hakuna kuchukuliwa mateka,
wala kilio cha taabu
katika barabara zetu.

15 [d]Heri watu ambao hili ni kweli;
heri wale ambao Bwana ni
Mungu wao.

### Zaburi 145[e]

*Wimbo Wa Kusifu Ukuu Na Wema Wa Mungu*

*Wimbo wa Sifa. Wa Daudi.*

1 [f]Nitakutukuza wewe, Mungu wangu
Mfalme,
nitalisifu jina lako milele na
milele.
2 [g]Kila siku nitakusifu
na kulitukuza jina lako milele na
milele.

3 [h]Bwana ni mkuu, anayestahili
kusifiwa sana,
ukuu wake haupimiki.
4 [i]Kizazi kimoja kitasifia kazi zako kwa
kizazi kingine,
watasimulia matendo yako makuu.
5 [j]Watasema juu ya utukufu wa fahari
ya ukuu wako,
nami nitatafakari juu ya kazi zako
za ajabu.
6 [k]Watasimulia uwezo wa kazi zako za
kutisha,
nami nitatangaza matendo yako
makuu.
7 [l]Wataadhimisha wema wako
mwingi,
na wataimba kwa shangwe juu ya
haki yako.

8 [m]Bwana ni mwenye neema na
mwingi wa huruma,
si mwepesi wa hasira, bali ni
mwingi wa upendo.
9 [n]Bwana ni mwema kwa wote,
ana huruma kwa vyote
alivyovifanya.
10 [o]Ee Bwana, vyote ulivyovifanya
vitakusifu,
watakatifu wako watakutukuza.
11 Watasimulia utukufu wa ufalme
wako
na kusema juu ya ukuu wako,
12 [p]ili watu wote wajue matendo yako
makuu
na utukufu wa fahari ya ufalme
wako.
13 [q]Ufalme wako ni ufalme wa milele,
mamlaka yako hudumu vizazi
vyote.

---

[a]**144:12** Za 92:12-14; 128:3; 4:4; 7:4
[b]**144:13** Mit 3:10
[c]**144:14** Mit 14:4; 2Fal 25:11; Isa 24:11; Yer 14:2-3; Law 26:17
[d]**144:15** Kum 28:3; 33:29
[e]1 Zaburi hii imetungwa kila mstari (ikiwa ni pamoja na 13b) ukianzia na herufi ya alfabeti ya Kiebrania zikifuatana tangu Aleph (A) hadi Taw (T); zote ni 22.
[f]**145:1** Za 30:1; 34:1; 2:6; 5:2; 54:6
[g]**145:2** Za 71:6; 34:1; Isa 25:1; 26:8
[h]**145:3** 2Sam 22:4; Ay 5:9; Za 95:3; 96:4
[i]**145:4** Za 22:30; 71:16; Kum 11:19
[j]**145:5** Za 96:6; 148:13; 75:1
[k]**145:6** Kum 32:3; Za 75:1; 78:4; 66:3; 106:2
[l]**145:7** Kut 18:9; Za 5:11; 27:13; 138:5; 101:1
[m]**145:8** Za 57:10; 86:15; 103:8; Kut 34:6; Hes 14:18; Yn 1:17; Mao 3:22
[n]**145:9** 1Nya 16:34; Mt 19:17; Nah 1:7; Mk 10:18; Mdo 14:17; Za 103:13, 14; 136:1; 100:5
[o]**145:10** Za 8:6; 103:22; 139:14; 148:14; 19:1; 149:9; 30:4; 115:17-18
[p]**145:12** Za 103:19; 105:1; 75:1; Isa 2:10, 19, 21
[q]**145:13** Kut 15:18; 1Tim 1:17; 2Pet 1:11; Ufu 11:15; Kum 7:9; 1Kor 1:9; Yos 23:14

BWANA ni mwaminifu kwa ahadi
zake zote
na mwenye upendo kwa vyote
alivyovifanya.
14 [a]BWANA huwategemeza wote
waangukao,
na huwainua wote waliolemewa
na mizigo yao.
15 [b]Macho yao wote yanakutazama
wewe,
nawe huwapa chakula chao wakati
wake.
16 [c]Waufumbua mkono wako,
watosheleza haja ya kila kitu
kilicho hai.

17 [d]BWANA ni mwenye haki katika njia
zake zote,
na mwenye upendo kwa vyote
alivyovifanya.
18 [e]BWANA yu karibu na wote
wamwitao,
karibu na wote wamwitao kwa
uaminifu.
19 [f]Huwatimizia wamchao matakwa
yao,
husikia kilio chao na kuwaokoa.
20 [g]BWANA huwalinda wote
wampendao,
bali waovu wote atawaangamiza.

21 [h]Kinywa changu kitazinena sifa za
BWANA.
Kila kiumbe na kilisifu jina lake
takatifu
milele na milele.

[a]**145:14** Za 37:17; 146:8; 38:6; 1Sam 2:8
[b]**145:15** Mwa 1:30; Ay 28:5; Mt 6:26; Za 37:25
[c]**145:16** Za 90:14; 104; 28
[d]**145:17** Kut 9:27; Ezr 9:15
[e]**145:18** Flp 4:5; Za 46:1; 18:6; 80:18; 91:1; Isa 61:10; Ufu 3:20; Yak 4:8; 1Yn 2:24; Yud 23; Yn 4:23; 14:23; Hes 23:21
[f]**145:19** 1Yn 5:14; Za 20:4; 31:22; 40:1; 7:10; 34:18; 1Sam 10:19; Ay 22:28
[g]**145:20** Za 94:23; 31:23; 91:14; 97:10; 1:6; 1Pet 1:5
[h]**145:21** Za 71:8; 65:2; 150:6; 30:4; 99:3; Kut 3:15

## Zaburi 146

*Kumsifu Mungu Mwokozi*

1 [i]Msifuni BWANA![j]

Ee nafsi yangu, umsifu BWANA,
2 [k]Nitamsifu BWANA maisha yangu
yote;
nitamwimbia Mungu wangu sifa
wakati wote niishipo.
3 [l]Usiweke tumaini lako kwa wakuu,
kwa wanadamu ambao hufa,
ambao hawawezi kuokoa.
4 [m]Roho yao itokapo hurudi
mavumbini,
siku hiyo hiyo mipango yao yote
hukoma.

5 [n]Heri yeye ambaye Mungu wa
Yakobo ni msaada wake,
ambaye tumaini lake ni katika
BWANA, Mungu wake,
6 [o]Muumba wa mbingu na nchi,
na bahari na vyote vilivyomo
ndani yake:
BWANA anayedumu kuwa
mwaminifu
milele na milele.
7 [p]Naye huwapatia haki walioonewa
na kuwapa wenye njaa chakula.
BWANA huwaweka wafungwa huru,
8 [q]BWANA huwafumbua vipofu
macho,
BWANA huwainua waliolemewa na
mizigo yao,
BWANA huwapenda wenye haki.

[i]**146:1** Za 103:1; 104:1
[j]1 Msifuni BWANA kwa Kiebrania ni Hallelu Yah.
[k]**146:2** Za 104:33; 63:4; 105:2
[l]**146:3** Za 118:9; 60:11; 108:12; Isa 2:22
[m]**146:4** Mhu 12:7; Mwa 3:19; Ay 7:21; 1Kor 2:6; Za 103:14; 33:10
[n]**146:5** Za 119:43; 37:9; 144:15; 33:18; 71:5; 70:5; 121:2; Yer 17:7
[o]**146:6** 2Nya 2:12; Za 18:25; 108:4; 117:2; 115:15; Mdo 14:15; Kum 7:9; Mik 7:20; Ufu 10:6; 14:7
[p]**146:7** Za 37:17; 103:6; 107:9; 145:15; 66:11; 68:6
[q]**146:8** Isa 32:3; 29:18; 35:5; 42:7, 18, 19; 43:8; Ay 23:10; Kut 4:11; Za 38:6; Kum 7:13; Mt 11:5; Mit 20:12

9 [a]BWANA huwalinda wageni
na kuwategemeza yatima na
wajane,
lakini hupinga njia za waovu.

10 [b]BWANA atamiliki milele,
Mungu wako, ee Sayuni,
kwa vizazi vyote.

Msifuni BWANA.

## Zaburi 147

*Kumsifu Mungu Mwenye Nguvu Zote*

1 [c]Msifuni BWANA.

Tazama jinsi ilivyo vyema
kumwimbia Mungu wetu sifa,
jinsi inavyopendeza na kustahili
kumsifu yeye!

2 [d]BWANA hujenga Yerusalemu,
huwakusanya Israeli walio
uhamishoni.
3 [e]Anawaponya waliovunjika mioyo
na kuvifunga vidonda vyao.

4 [f]Huzihesabu nyota
na huipa kila moja jina lake.
5 [g]Bwana wetu ni mkuu na mwenye
uwezo mwingi,
ufahamu wake hauna kikomo.
6 [h]BWANA huwahifadhi wanyenyekevu
lakini huwashusha waovu mpaka
mavumbini.

7 [i]Mwimbieni BWANA kwa shukrani,
mpigieni Mungu wetu kinubi.
8 [j]Yeye huzifunika anga kwa mawingu,
huinyeshea ardhi mvua,
na kuzifanya nyasi kuota juu ya
vilima.
9 [k]Huwapa chakula mifugo
na pia makinda ya kunguru
yanapolia.

10 [l]Furaha yake haipo katika nguvu za
farasi,
wala furaha yake kwenye miguu
ya mwanadamu.
11 [m]BWANA hupendezwa na wale
wamchao,
wale wanaoweka tumaini
lao katika upendo wake
usiokoma.

12 [n]Mtukuze BWANA, ee Yerusalemu,
msifu Mungu wako, ee Sayuni,
13 [o]kwa maana huimarisha makomeo ya
malango yako
na huwabariki watu wako walio
ndani yako.
14 [p]Huwapa amani mipakani mwenu
na kukushibisha kwa ngano safi
kabisa.

15 [q]Hutuma amri yake duniani,
neno lake hukimbia kasi.
16 [r]Anatandaza theluji kama sufu
na kutawanya umande kama
majivu.
17 [s]Huvurumisha mvua yake ya mawe
kama changarawe.
Ni nani awezaye kustahimili ukali
wa baridi yake?

---

[a]**146:9** Law 19:34; Za 10:18; Kut 22:22; Yak 1:27
[b]**146:10** Mwa 21:33; 1Nya 16:31; Za 93:1; 99:1; Ufu 11:15
[c]**147:1** Za 135:3; 33:1
[d]**147:2** Za 51:18; 106:47; Kum 30:3; Isa 27:13; Yer 32:37; Eze 36:24
[e]**147:3** Za 34:18; Isa 1:6; 61:1; Eze 34:16; Ebr 12:13; Ay 5:18; Lk 4:18
[f]**147:4** Mwa 15:5; Isa 40:26
[g]**147:5** Kut 14:31; Nah 1:3; 1Nya 16:25; Za 48:1; 145:3; Isa 40:28
[h]**147:6** 2Nya 33:23; Za 146:8, 9; 37:9, 10; 145:20
[i]**147:7** Za 30:4; 33:3; 42:4; 27:6; 98:5; Efe 2:20
[j]**147:8** Kum 32:2; 11:14; 2Sam 1:21; Ay 26:8; 38:26; 5:10; 28:26; Za 104:14
[k]**147:9** Ay 38:41; Mt 6:26; Mwa 8:7; 1:30; Lk 12:24; Za 104:27, 28
[l]**147:10** 1Sam 16:7; Hos 1:7; Ay 39:11; Za 33:16-17
[m]**147:11** Za 35:27; 33:18; 103:11; 119:43; 6:4
[n]**147:12** Za 48:1
[o]**147:13** Kum 33:25; Law 25:21; Za 128:5; 134:3
[p]**147:14** Law 26:6; 2Sam 7:10; Isa 48:18; Za 132:15; Kum 32:14
[q]**147:15** Ay 37:12; Za 33:9; 148:5; Isa 55:11
[r]**147:16** Za 148:8; Ay 37:12; 38:29
[s]**147:17** Kut 9:22, 23; Ay 38:22; Za 78:47

18 [a]Hutuma neno lake na kuviyeyusha,
huvumisha upepo wake, nayo maji
hutiririka.

19 [b]Amemfunulia Yakobo neno lake,
sheria zake na maagizo yake kwa
Israeli.
20 [c]Hajafanya hivyo kwa taifa lingine
lolote,
hawazijui sheria zake.

Msifuni BWANA.

## Zaburi 148

*Mwito Kwa Ulimwengu Kumsifu Mungu*

1 [d]Msifuni BWANA.

Msifuni BWANA kutoka mbinguni,
msifuni juu vileleni.
2 [e]Msifuni, enyi malaika wake wote,
msifuni yeye, enyi jeshi lake lote
la mbinguni.
3 [f]Msifuni yeye, enyi jua na mwezi,
msifuni yeye, enyi nyota zote
zing'aazo.
4 [g]Msifuni yeye, enyi mbingu zilizo juu
sana,
na ninyi maji juu ya anga.
5 [h]Vilisifu jina la BWANA
kwa maana aliamuru navyo
vikaumbwa.
6 [i]Aliviweka mahali pake milele na
milele,
alitoa amri ambayo haibadiliki
milele.

7 [j]Mtukuzeni BWANA kutoka duniani,
ninyi viumbe vikubwa vya
baharini na vilindi vyote vya
bahari,
8 [k]umeme wa radi na mvua ya mawe,
theluji na mawingu,
pepo za dhoruba zinazofanya amri
zake,
9 [l]ninyi milima na vilima vyote,
miti ya matunda na mierezi yote,
10 [m]wanyama wa mwituni na mifugo
yote,
viumbe vidogo na ndege warukao,
11 [n]wafalme wa dunia na mataifa yote,
ninyi wakuu na watawala wote wa
dunia,
12 wanaume vijana na wanawali,
wazee na watoto.

13 [o]Wote na walisifu jina la BWANA,
kwa maana jina lake pekee
limetukuka,
utukufu wake uko juu ya nchi na
mbingu.
14 [p]Amewainulia watu wake pembe,[q]
sifa ya watakatifu wake wote,
ya Israeli, watu walio karibu na
moyo wake.

Msifuni BWANA.

## Zaburi 149

*Wimbo Wa Kumsifu Mungu Kwa Wema Wake*

1 [r]Msifuni BWANA.

Mwimbieni BWANA wimbo mpya,
sifa zake katika kusanyiko la
watakatifu.

---

[a]**147:18** Za 33:9; 107:20; 50:3
[b]**147:19** Kut 20:1; Mal 4:4; Za 78:5; Yos 1:8; Kum 33:4; 2Fal 22:8; Rum 3:2; 9:4
[c]**147:20** Rum 3:1-2; Kum 4:7-8, 32-34; Za 79:6; 103:1; 33:2; Mdo 14:16
[d]**148:1** Za 33:2; 103; 1; 19:1; 69:34; 150:1
[e]**148:2** Za 103:20; 1Fal 22:19; Dan 7:10; Ebr 1:7
[f]**148:3** Za 19:1
[g]**148:4** Kum 10:14; Mwa 1:7; 1Fal 8:27
[h]**148:5** Za 145:21; 147:15; Ebr 11:3
[i]**148:6** Yer 31:35-36; 33:25; 33:25
[j]**148:7** Za 33:2; 74:13, 14; Mwa 1:21; Isa 43:20; Kum 33:13
[k]**148:8** Yos 10:11; Ay 37:11, 12; Za 147:15-18; 103:20; Kut 9:18
[l]**148:9** Isa 44:23; 49:13; 55:12
[m]**148:10** Isa 43:20; Hos 2:18
[n]**148:11** Za 102:15; Mdo 17:28
[o]**148:13** Za 113:2; 138:4; 145:5; 8:1; Isa 6:3; Flp 2:9
[p]**148:14** Kut 15:2; 1Pet 2:9; Za 22:3; 145:10; Kum 26:19; Efe 2:17; 1Sam 1:2
[q]14 Pembe hapa inawakilisha mwenye nguvu, yaani mfalme.
[r]**149:1** Za 33:2; 103:1; 28:7; 1:5; 96:1; Ufu 5:9; Isa 42:10

2 [a]Israeli na washangilie katika
Muumba wao,
watu wa Sayuni na wafurahi
katika Mfalme wao.
3 [b]Na walisifu jina lake kwa kucheza
na wampigie muziki kwa matari
na kinubi.
4 [c]Kwa maana BWANA anapendezwa
na watu wake,
anawavika wanyenyekevu taji ya
wokovu.
5 [d]Watakatifu washangilie katika
heshima hii,
na waimbe kwa shangwe
vitandani mwao.

6 [e]Sifa za Mungu na ziwe vinywani
mwao
na upanga ukatao kuwili mikononi
mwao,
7 [f]ili walipize mataifa kisasi
na adhabu juu ya mataifa,
8 [g]wawafunge wafalme wao kwa
minyororo,
wakuu wao kwa pingu za chuma,
9 [h]ili kuwafanyia hukumu
iliyoandikwa dhidi yao.
Huu ndio utukufu wa watakatifu
wake wote.

Msifuni BWANA.

## Zaburi 150

*Msifuni BWANA Kwa Ukuu Wake*

1 [i]Msifuni BWANA.

Msifuni Mungu katika patakatifu
pake,
msifuni katika mbingu zake kuu.
2 [j]Msifuni kwa matendo yake makuu,
msifuni kwa kadiri ya wingi wa
ukuu wake.
3 [k]Msifuni kwa mvumo wa tarumbeta,
msifuni kwa kinubi na zeze,
4 [l]msifuni kwa matari na kucheza,
msifuni kwa kinanda cha nyuzi na
filimbi,
5 [m]msifuni kwa matoazi yaliayo,
msifuni kwa matoazi yavumayo
sana.

6 [n]Kila chenye pumzi na kimsifu
BWANA.

Msifuni BWANA!

---

[a]**149:2** Yer 51:48; Zek 9:9; Za 10:16; 47:6; 95:6; Ay 35:10; 10:3; Isa 13:3; 32:1; 44:2; 45:11; 54:5
[b]**149:3** Kut 15:20; Za 57:8
[c]**149:4** Za 35:27; 147:11; 132:16; Mit 11:20
[d]**149:5** Za 132:16; 42:8; Ay 35:10
[e]**149:6** Za 66:17; Ebr 4:12; Ufu 1:16; Neh 4:17; Kum 7:1, 2
[f]**149:7** Hes 31:3; Kum 32:41; Za 81:15
[g]**149:8** 2Sam 3:34; Isa 14:1-2; 2Nya 33:11
[h]**149:9** Kum 7:1; 1Yn 5:4; Eze 28:26; Za 145:10; Rum 16:20
[i]**150:1** Za 112:1; 73:17; 68:24-26; 102:19; 148:1
[j]**150:2** Kum 3:24; Kut 15:7
[k]**150:3** Hes 10:2; Za 57:8
[l]**150:4** Kut 15:20; Za 45:8; Isa 38:20; Mwa 4:21
[m]**150:5** 2Sam 6:5
[n]**150:6** Za 103:22; Ufu 5:13

# MITHALI

*Utangulizi: Kusudi Na Kiini*

1 [a]Mithali za Solomoni mwana wa Daudi, mfalme wa Israeli:

2 Kwa kupata hekima na nidhamu;
kwa kufahamu maneno ya busara;
3 [b]kwa kujipatia nidhamu na busara,
kufanya lililo sawa, haki na bila kupendelea;
4 [c]huwapa busara wajinga,
maarifa na akili kwa vijana;
5 [d]wenye hekima na wasikilize nao waongeze elimu yao,
wenye kupambanua na wapate mwongozo;
6 [e]kwa kufahamu mithali na mifano,
misemo na vitendawili vya wenye hekima.

7 [f]Kumcha BWANA ndicho chanzo cha maarifa,
lakini wapumbavu hudharau hekima na adabu.

*Onyo Dhidi Ya Ushawishi Wa Marafiki Waovu*

8 [g]Mwanangu, sikiliza mwongozo wa baba yako,
wala usiyaache mafundisho ya mama yako.
9 [h]Hayo yatakuwa taji la maua la neema kichwani pako,
na mkufu wa kuipamba shingo yako.

10 [i]Mwanangu, kama wenye dhambi wakikushawishi,
usikubaliane nao.
11 [j]Kama wakisema, "Twende tufuatane;
tukamvizie mtu na kumwaga damu,
njoo tukavizie nafsi isiyo na hatia;
12 [k]tuwameze wakiwa hai kama kaburi,[l]
wakiwa wazima kama wale wanaotumbukia shimoni.
13 Tutapata aina zote za vitu vya thamani
na kujaza nyumba zetu kwa nyara.
14 [m]Njoo ushirikiane nasi,
vitu vyote tutakavyopata tutagawana."
15 [n]Mwanangu, usiandamane nao.
Usiweke mguu wako katika njia zao,
16 [o]kwa kuwa miguu yao hukimbilia kwenye dhambi,
ni wepesi kumwaga damu.
17 Tazama ni jinsi gani ilivyo kazi bure kutandaza wavu
wakati ndege wote wanakuona!
18 [p]Watu hawa huvizia kumwaga damu yao wenyewe;
hujivizia tu wenyewe!
19 [q]Huu ndio mwisho wa wote ambao wanajipatia mali kwa hila;
huuondoa uhai wa wale wenye mali.

*Onyo Dhidi Ya Kukataa Hekima*

20 [r]Hekima huita kwa sauti kuu barabarani,
hupaza sauti yake kwenye viwanja vikubwa;

---

[a]**1:1** 1Fal 4:29-34
[b]**1:3** Mit 2:1; 2:1, 9
[c]**1:4** Mit 8:5, 12; 2:10-11
[d]**1:5** Mit 9:9
[e]**1:6** Za 78:2; Mt 13:10-17; Hes 12:8; Amu 14:12
[f]**1:7** Kut 20:20; Ay 28:28
[g]**1:8** Mit 6:20; 22:17; Kum 21:18
[h]**1:9** Mit 3:21-22; 4:1-9
[i]**1:10** Mwa 39:7; Ay 24:15; Kum 13:8; Rum 16:18
[j]**1:11** Mit 12:6; Yer 5:26; Mik 7:2
[k]**1:12** Ay 33:18; Mwa 38:25; Za 40:3
[l]12 Kaburi hapa maana yake ni Kuzimu, kwa Kiebrania ni Sheol.
[m]**1:14** Mit 1:19
[n]**1:15** Za 119:101; Mwa 49:6; Mit 4:14
[o]**1:16** Mit 6:18; Isa 59:7
[p]**1:18** Za 71:10
[q]**1:19** Mit 11:19; 15:27; 2Fal 5:20-27
[r]**1:20** Ay 28:12; Mt 7:10-13; 9:1-3, 13-15

21 kwenye makutano ya barabara za mji
zenye makelele mengi hupaza sauti,
kwenye malango ya mji hutoa hotuba yake:

22 [a]"Enyi wajinga, mtang'ang'ania ujinga wenu hadi lini?
Mpaka lini wenye mizaha watafurahia mizaha,
na wapumbavu kuchukia maarifa?
23 [b]Kama mngekuwa mmeitikia karipio langu,
ningekuwa nimemimina roho yangu kwenu
na kuwafahamisha maneno yangu.
24 [c]Lakini kwa kuwa mlinikataa nilipowaita
na hakuna yeyote aliyekubali
niliponyoosha mkono wangu,
25 [d]kwa kuwa mliyapuuza mashauri yangu yote
na hamkukubali karipio langu,
26 [e]mimi nami nitawacheka katika maafa yenu,
nitawadhihaki wakati janga litawapata:
27 [f]wakati janga litawapata kama tufani,
wakati maafa yatawazoa kama upepo wa kisulisuli,
wakati dhiki na taabu zitawalemea.

28 [g]"Ndipo watakaponiita lakini sitawajibu;
watanitafuta lakini hawatanipata.
29 [h]Kwa kuwa walichukia maarifa,
wala hawakuchagua kumcha Bwana,
30 [i]kwa kuwa hawakukubali mashauri yangu,
na kukataa maonyo yangu,
31 [j]watakula matunda ya njia zao,
na watashibishwa matunda ya hila zao.
32 [k]Kwa kuwa ukaidi wa wajinga utawaua,
nako kuridhika kwa wajinga kutawaangamiza.
33 [l]Lakini yeyote anisikilizaye ataishi kwa usalama,
atatulia, bila kuwa na hofu ya madhara."

*Faida Za Hekima*

2 [m]Mwanangu, kama utayakubali maneno yangu
na kuyaweka akiba maagizo yangu ndani mwako,
2 [n]kutega sikio lako kwenye hekima
na kuweka moyo wako katika ufahamu,
3 [o]na kama ukiita busara
na kuita kwa sauti ufahamu,
4 [p]na kama utaitafuta kama fedha
na kuitafuta sana kama hazina iliyofichwa,
5 [q]ndipo utakapoelewa kumcha Bwana
na kupata maarifa ya Mungu.
6 [r]Kwa maana Bwana hutoa hekima,
na kinywani mwake hutoka maarifa na ufahamu.
7 [s]Anahifadhi ushindi kwa ajili ya mwadilifu,
yeye ni ngao kwa wale wasio na lawama,

---

[a]**1:22** Mit 6:32; 7:7; 8:5; 9:4, 16; Za 50:17
[b]**1:23** Yoe 2:28; Yn 7:37
[c]**1:24** Isa 65:12; Zek 7:11
[d]**1:25** Lk 7:30
[e]**1:26** Za 2:4; Kum 28:63; Mit 10:24
[f]**1:27** Za 18:18; Mit 5:12-14
[g]**1:28** Isa 1:15; Mik 3:4; Eze 8:18; Hos 5:6
[h]**1:29** Ay 21:14; Isa 27:11; Mdo 7:51
[i]**1:30** Ay 21:14; Za 81:11
[j]**1:31** 2Nya 36:16; Yer 14:16
[k]**1:32** Isa 66:4; Yer 2:19
[l]**1:33** Hes 24:21; Za 25:12; 112:8
[m]**2:1** Mit 1:8
[n]**2:2** Mit 22:17
[o]**2:3** Yak 1:5
[p]**2:4** Ay 3:21; Mt 13:44; 6:19-21
[q]**2:5** Kum 4:6
[r]**2:6** Ay 12:13; Lk 21:15; Yak 1:5
[s]**2:7** Mwa 6:9; 15:1; Mit 30:5-6; Za 84:11

8 [a]kwa kuwa hulinda mwenendo wa mwenye haki
na kuhifadhi njia ya waaminifu wake.

9 [b]Ndipo utafahamu lipi lililo kweli na haki
na sawa: yaani kila njia nzuri.
10 [c]Kwa maana hekima itaingia moyoni mwako,
nayo maarifa yataifurahisha nafsi yako.
11 [d]Busara itakuhifadhi
na ufahamu utakulinda.

12 [e]Hekima itakuokoa kutoka njia za waovu,
kutoka kwa watu ambao maneno yao yamepotoka,
13 [f]wale waachao mapito yaliyonyooka
wakatembea katika njia za giza,
14 [g]wale wapendao kutenda mabaya
na kufurahia upotovu wa ubaya,
15 [h]ambao mapito yao yamepotoka
na ambao ni wapotovu katika njia zao.

16 [i]Itakuokoa pia kutokana na mwanamke kahaba,
kutokana na mke aliyepotoka mwenye maneno
ya kushawishi kutenda ubaya,
17 [j]aliyemwacha mwenzi wa ujana wake
na kupuuza agano alilofanya mbele ya Mungu.
18 [k]Kwa maana nyumba yake huelekea kwenye kifo
na mapito yake kwenye roho za waliokufa.
19 [l]Hakuna yeyote aendaye kwake akarudi,
au kufikia mapito ya uzima.

20 [m]Hivyo utatembea katika njia za watu wema
na kushikamana na mapito ya wenye haki.
21 [n]Kwa maana wanyofu wataishi katika nchi,
nao wasio na lawama watabakia ndani yake.
22 [o]Bali waovu watakatiliwa mbali kutoka nchi,
nao wasio waaminifu watang'olewa kutoka humo.

*Faida Nyingine Za Hekima*

3 [p]Mwanangu, usisahau mafundisho yangu,
bali zitunze amri zangu moyoni mwako,
2 [q]kwa kuwa zitakuongezea miaka mingi ya maisha yako
na kukuletea mafanikio.

3 [r]Usiache kamwe upendo na uaminifu vitengane nawe;
vifunge shingoni mwako,
viandike katika ubao wa moyo wako.
4 [s]Ndipo utapata kibali na jina zuri
mbele za Mungu na mwanadamu.

5 [t]Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote
wala usizitegemee akili zako mwenyewe;
6 [u]katika njia zako zote mkiri yeye,
naye atayanyoosha mapito yako.

[a]**2:8** 1Sam 2:9; Za 18:25
[b]**2:9** Kum 1:16
[c]**2:10** Mit 14:33
[d]**2:11** Mit 4:6
[e]**2:12** Mit 2:16; 3:13-18; 4:5
[f]**2:13** Mit 4:19; Yn 3:19; Efe 4:18
[g]**2:14** Mit 15:21; Yer 11:15
[h]**2:15** Za 125:5; Mit 21:8
[i]**2:16** Mit 6:20-29; 7:5-27
[j]**2:17** Mal 2:14; Mwa 2:24
[k]**2:18** Mit 5:5; 7:27; 9:18
[l]**2:19** Mit 5:8; Mhu 7:26; Ebr 13:4
[m]**2:20** Ebr 6:12
[n]**2:21** Za 37:29
[o]**2:22** Ay 18:17; Za 37:38; Kum 29:28
[p]**3:1** Kum 30:16; Za 44:17; Mit 4:5
[q]**3:2** Mit 9:6; 4:10
[r]**3:3** Kum 6:8; Mit 6:21; 2Kor 3:3
[s]**3:4** 1Sam 2:26; Lk 2:52; Mdo 2:47
[t]**3:5** Za 4:5; Yer 9:23
[u]**3:6** 1Nya 28:9; Ay 33:11; Yer 42:3

[7] [a]Usiwe mwenye hekima machoni
pako mwenyewe;
mche BWANA ukajiepushe na
uovu.
[8] [b]Hii itakuletea afya mwilini mwako,
na mafuta kwenye mifupa yako.

[9] [c]Mheshimu BWANA kwa mali zako
na
kwa malimbuko ya mazao yako
yote;
[10] [d]ndipo ghala zako zitakapojaa hadi
kufurika,
viriba vyako vitafurika kwa
mvinyo mpya.

[11] [e]Mwanangu, usiidharau adhabu ya
BWANA
na usichukie kukaripiwa naye,
[12] [f]kwa sababu BWANA huwaadibisha
wale awapendao,
kama vile baba afanyavyo
kwa mwana apendezwaye naye.

[13] [g]Heri mtu yule aonaye hekima,
mtu yule apataye ufahamu,
[14] [h]kwa maana hekima ana faida kuliko
fedha
na mapato yake ni bora kuliko ya
dhahabu safi.
[15] [i]Hekima ana thamani kuliko
marijani;
hakuna chochote unachokitamani
kinachoweza kulinganishwa naye.
[16] [j]Maisha marefu yako katika mkono
wake wa kuume;
katika mkono wake wa kushoto
kuna utajiri na heshima.
[17] [k]Njia zake zinapendeza,
mapito yake yote ni amani.
[18] [l]Yeye ni mti wa uzima kwa wale
wanaomkumbatia;
wale wamshikao watabarikiwa.

[19] [m]Kwa hekima BWANA aliiweka
misingi ya dunia,
kwa ufahamu aliziweka mbingu
mahali pake;
[20] [n]kwa maarifa yake vilindi
viligawanywa,
nayo mawingu yanadondosha
umande.

[21] [o]Mwanangu, hifadhi maamuzi mema
na busara,
usiache vitoke machoni pako;
[22] [p]ndipo vitakapokuwa uzima nafsini
mwako
na pambo la neema shingoni
mwako.
[23] Kisha utaenda katika njia yako
salama,
wala mguu wako hautajikwaa;
[24] [q]ulalapo, hautaogopa;
ulalapo usingizi wako utakuwa
mtamu.

[25] [r]Usiogope maafa ya ghafula
au maangamizi yanayowapata
waovu,
[26] [s]kwa kuwa BWANA atakuwa tumaini
lako
na kuepusha mguu wako kunaswa
katika mtego.

[27] [t]Usizuie wema kwa wale
wanaostahili
ikiwa katika uwezo wako kutenda.

---

[a]**3:7** Isa 5:21; Rum 12:16; Kum 4:6
[b]**3:8** Za 38:3; Mit 4:22; Ay 21:24
[c]**3:9** Kut 23:19; 26:1-15
[d]**3:10** Kum 28:8; Za 144:13; Ay 22:21; Mal 3:10-12
[e]**3:11** Mit 1:8-9; Ay 5:17
[f]**3:12** Mit 13:24; Ufu 3:19; Ay 3:19; 5:17; Ebr 12:5-6
[g]**3:13** Mit 8:34, 35
[h]**3:14** Ay 28:15; Mit 16:16
[i]**3:15** Ay 28:17-19
[j]**3:16** 1Fal 3:13-14; Mit 8:18
[k]**3:17** Mit 16:7; Mt 11:28-30
[l]**3:18** Mwa 2:9; Ufu 2:7
[m]**3:19** Ay 28:25-27; Za 104:24; Mit 8:27-29
[n]**3:20** Kum 33:28; Ay 36:28
[o]**3:21** Mit 1:8-9; 6:20; 4:20-22
[p]**3:22** Kum 30:20; Mit 4:20-22
[q]**3:24** Law 26:6; Za 3:5; Ay 11:18; Yer 31:25
[r]**3:25** Za 91:5; 112:7
[s]**3:26** 1Sam 2:9
[t]**3:27** Rum 13:7; Gal 6:10

28 [a]Usimwambie jirani yako,
“Njoo baadaye, nitakupa kesho”:
wakati wewe unacho kitu kile
karibu nawe.

29 [b]Usifanye hila ya kumdhuru jirani
yako,
ambaye anaishi karibu na wewe
akikuamini.
30 [c]Usimshtaki mtu bila sababu,
wakati hajakutenda dhara lolote.

31 [d]Usimwonee wivu mtu mwenye jeuri
wala kuchagua njia yake iwayo
yote,
32 [e]kwa kuwa Bwana humchukia mtu
mpotovu,
lakini siri yake iko kwa mwenye
haki.

33 [f]Laana ya Bwana i juu ya nyumba
ya mwovu,
lakini yeye huibariki nyumba ya
mwenye haki.
34 [g]Huwadhihaki wale wanaodhihaki,
lakini huwapa neema wale
wanyenyekevu.
35 Wenye hekima hurithi heshima,
bali huwaaibisha wapumbavu.

*Hekima Ni Bora Kupita Vitu Vyote*

4 [h]Sikilizeni wanangu, mafundisho ya
baba yenu;
sikilizeni kwa makini na mpate
ufahamu.
2 Ninawapa mafundisho ya maana,
kwa hiyo msiyaache mafundisho
yangu.
3 [i]Nilipokuwa mvulana mdogo katika
nyumba ya baba yangu,
ningali mchanga na mtoto pekee
kwa mama yangu,
4 [j]baba alinifundisha akisema,
“Yashike maneno yangu yote kwa
moyo wako wote;
yashike maagizo yangu na wewe
utaishi.
5 [k]Pata hekima, pata ufahamu;
usiyasahau maneno yangu wala
usiyaache.
6 [l]Usimwache hekima naye atakuweka
salama;
mpende, naye atakulinda.
7 [m]Hekima ni bora kuliko vitu vyote;
kwa hiyo jipe hekima.
Hata ikikugharimu vyote ulivyo
navyo, pata ufahamu.
8 [n]Mstahi, naye atakukweza;
mkumbatie, naye atakuheshimu.
9 [o]Atakuvika shada la neema kichwani
mwako
na kukupa taji ya utukufu.”

10 [p]Sikiliza mwanangu, kubali
ninachokuambia,
nayo miaka ya maisha yako
itakuwa mingi.
11 [q]Ninakuongoza katika njia ya hekima
na kukuongoza katika mapito
yaliyonyooka.
12 [r]Utembeapo, hatua zako
hazitazuiliwa;
ukimbiapo, hutajikwaa.
13 [s]Mkamate sana elimu, usimwache
aende zake;
mshike, maana yeye ni uzima
wako.
14 [t]Usiuweke mguu wako katika njia ya
waovu
wala usitembee katika njia ya
watu wabaya.

---

[a]**3:28** Law 19:13; Lk 10:25-37; Kum 24:15
[b]**3:29** Zek 8:17
[c]**3:30** Rum 12:18
[d]**3:31** Za 37:1; Mit 24:1-2
[e]**3:32** Za 101:4; Ay 29:4
[f]**3:33** Ay 5:3; Mal 2:2; Zek 5:4
[g]**3:34** Za 18:25-27; Mt 23:12
[h]**4:1** Mit 1:8; 19:20; Ay 8:10
[i]**4:3** 1Nya 29:1; 2Sam 12:24
[j]**4:4** Mit 7:2; 1Nya 28:9
[k]**4:5** Mit 3:13-18; 16:16
[l]**4:6** 2The 2:10; Mit 2:11
[m]**4:7** Mt 13:44-46; Mit 23:23
[n]**4:8** 1Sam 2:30; Mit 3:18
[o]**4:9** Mit 1:8-9
[p]**4:10** Kum 11:21; Mit 3:2
[q]**4:11** 1Sam 12:23; 2Sam 22:37; Za 5:8
[r]**4:12** Ay 18:7; Yer 13:16; Za 18:36
[s]**4:13** Mit 3:22
[t]**4:14** Za 1:1; Mit 1:15

15 Epukana nayo, usisafiri katika njia hiyo;
achana nayo, na uelekee njia yako.
16 [a]Kwa kuwa hawawezi kulala mpaka watende uovu;
wanashindwa hata kusinzia mpaka wamwangushe mtu.
17 [b]Wanakula mkate wa uovu,
na kunywa mvinyo wa jeuri.

18 [c]Njia ya wenye haki ni kama nuru ya kwanza ya mapambazuko,
ambayo hung'aa zaidi na zaidi mpaka mchana mkamilifu.
19 [d]Lakini njia ya waovu ni kama giza nene;
hawajui kinachowafanya wajikwae.

20 [e]Mwanangu, yasikilize kwa makini yale ninayokuambia;
sikiliza kwa makini maneno yangu.
21 [f]Usiruhusu yaondoke machoni pako,
yahifadhi ndani ya moyo wako;
22 [g]kwa sababu ni uzima kwa wale wanaoyapata
na afya kwa mwili wote wa mwanadamu.
23 [h]Zaidi ya yote, linda moyo wako,
kuliko yote uyalindayo,
maana ndiko zitokako chemchemi za uzima.
24 Epusha kinywa chako na ukaidi;
weka mazungumzo machafu mbali na midomo yako.
25 [i]Macho yako na yatazame mbele,
kaza macho yako moja kwa moja mbele yako.
26 [j]Sawazisha mapito ya miguu yako
na njia zako zote ziwe zimethibitika.
27 [k]Usigeuke kulia wala kushoto;
epusha mguu wako na ubaya.

*Onyo Dhidi Ya Uzinzi*

5 [l]Mwanangu, sikiliza kwa makini hekima yangu,
sikiliza vizuri maneno yangu ya busara,
2 [m]ili uweze kutunza busara
na midomo yako ihifadhi maarifa.
3 [n]Kwa maana midomo ya mwanamke kahaba
hudondoza asali,
na maneno ya kinywa chake
ni laini kuliko mafuta;
4 [o]lakini mwisho wake ni mchungu kama nyongo,
mkali kama upanga ukatao kuwili.
5 [p]Miguu yake hushuka kuelekea kwenye kifo;
hatua zake huelekea moja kwa moja kaburini.[q]
6 [r]Yeye hafikiri juu ya njia ya uzima;
njia zake zimepotoka, lakini yeye hajui.

7 [s]Sasa basi wanangu, nisikilizeni;
msiache ninalowaambia.
8 [t]Njia zenu ziwe mbali naye,
msiende karibu na mlango wa nyumba yake,
9 usije ukatoa nguvu zako nzuri kwa wengine
na miaka yako kwa aliye mkatili,

[a]**4:16** Za 36:4; Mik 7:3
[b]**4:17** Mwa 49:5; Za 73:6; Mit 1:10-19; Isa 59:6; Yer 22:3; Hab 1:2; Mal 2:16
[c]**4:18** Mt 5:14; Ay 17:9; Isa 26:7; Dan 12:3; Yn 8:12
[d]**4:19** Ay 18:5; Yn 12:35
[e]**4:20** Za 34:11-16; Mit 1:8-9; 5:1
[f]**4:21** Mit 3:21
[g]**4:22** Mit 3:8
[h]**4:23** Mit 10:11; Mt 12:34
[i]**4:25** Ay 31:1
[j]**4:26** Ebr 12:13
[k]**4:27** Law 10:11; Kum 28:14
[l]**5:1** Mit 1:8
[m]**5:2** Mwa 2:7
[n]**5:3** Za 55:21; Mit 2:16
[o]**5:4** Mhu 7:26; Ebr 4:12
[p]**5:5** Za 9:17; Mit 2:18
[q]5 Kaburini hapa maana yake ni Kuzimu, kwa Kiebrania ni Sheol.
[r]**5:6** Mit 9:13; 30:20
[s]**5:7** Mit 1:8-9
[t]**5:8** Mit 6:20-29; 7:1-27

10 [a]wageni wasije wakasherehekea
utajiri wako
na jitihada yako ikatajirisha
nyumba ya mwanaume mwingine.
11 Mwishoni mwa maisha yako utalia
kwa uchungu,
wakati nyama na mwili wako
vimechakaa.
12 Utasema, "Tazama jinsi gani
nilivyochukia adhabu!
Tazama jinsi moyo wangu
ulivyodharau maonyo!
13 Sikuwatii walimu wangu
wala kuwasikiliza wakufunzi
wangu.
14 [b]Nimefika ukingoni mwa
maangamizi kabisa
katikati ya kusanyiko lote."

15 Kunywa maji kutoka kwenye kisima
chako mwenyewe,
maji yanayotiririka kutoka kwenye
kisima chako mwenyewe.
16 Je, chemchemi zako zifurike katika
barabara za mji
na vijito vyako vya maji
viwanjani?
17 Na viwe vyako mwenyewe,
kamwe visishirikishwe wageni.
18 [c]Chemchemi yako na ibarikiwe
na umfurahie mke wa ujana wako.
19 [d]Kulungu jike apendaye, kulungu
mzuri:
matiti yake na yakutosheleze siku
zote,
nawe utekwe daima na upendo
wake.
20 [e]Kwa nini mwanangu, utekwe na
mwanamke kahaba?
Kwa nini ukumbatie kifua cha mke
wa mwanaume mwingine?
21 [f]Kwa maana njia za mtu ni wazi
kabisa mbele za Bwana,
naye huyapima mapito yake yote.
22 [g]Matendo mabaya ya mtu mwovu
humnasa yeye mwenyewe;
kamba za dhambi yake
humkamata kwa nguvu.
23 [h]Atakufa kwa kukosa nidhamu,
akipotoshwa kwa upumbavu wake
mwenyewe.

*Maonyo Dhidi Ya Upumbavu*

6 [i]Mwanangu, kama umekuwa
mdhamini wa jirani yako,
ikiwa umeshika mikono kwa
kuweka ahadi
kwa ajili ya mwingine,
2 kama umetegwa na ulichosema,
umenaswa kwa maneno ya kinywa
chako,
3 basi fanya hivi mwanangu, ili
ujiweke huru,
kwa kuwa umeanguka mikononi
mwa jirani yako:
Nenda ukajinyenyekeshe kwake;
msihi jirani yako!
4 [j]Usiruhusu usingizi machoni pako,
usiruhusu kope zako zisinzie.
5 [k]Jiweke huru, kama swala mkononi
mwa mwindaji,
kama ndege kutoka kwenye mtego
wa mwindaji.

6 [l]Ewe mvivu, mwendee mchwa;
zitafakari njia zake ukapate
hekima!
7 Kwa maana yeye hana msimamizi,
wala mwangalizi, au mtawala,
8 [m]lakini hujiwekea akiba wakati wa
kiangazi
na hukusanya chakula chake
wakati wa mavuno.

[a]**5:10** Mit 29:3
[b]**5:14** Mit 1:24-27; 6:33; 31:3
[c]**5:18** Wim 4:12-15; Kum 20:7; Mal 2:14
[d]**5:19** Wim 2:9; 8:14
[e]**5:20** Mit 2:16; 7:5
[f]**5:21** Za 119:168; Hos 7:2; Yer 16:17; Ay 10:4; Ebr 4:13
[g]**5:22** Za 9:16; Hes 32:23; Ay 18:9
[h]**5:23** Ay 4:21; 36:12
[i]**6:1** Mwa 43:9; Ebr 7:22; Ezr 10:27; Mit 17:18
[j]**6:4** Rut 3:18; Za 132:4
[k]**6:5** Za 91:3; 2Sam 2:18; Isa 13:14; Za 91:3
[l]**6:6** Mit 6:11
[m]**6:8** Mit 30:24-25; 10:4

9 [a]Ewe mvivu, utalala hata lini?
Utaamka lini kutoka usingizi wako?
10 [b]Bado kulala kidogo, kusinzia kidogo,
bado kukunja mikono kidogo upate kupumzika:
11 [c]hivyo umaskini utakuja juu yako kama mnyang'anyi,
na kupungukiwa kutakujia kama mtu mwenye silaha.

12 Mtu mbaya sana na mlaghai,
ambaye huzungukazunguka
na maneno ya upotovu,
13 [d]ambaye anakonyeza kwa jicho lake,
anayetoa ishara kwa miguu yake
na kuashiria kwa vidole vyake,
14 [e]ambaye hupanga ubaya
kwa udanganyifu moyoni mwake:
daima huchochea fitina.
15 Kwa hiyo maafa yatamkumba ghafula;
ataangamizwa mara, pasipo msaada.

16 [f]Kuna vitu sita anavyovichukia Bwana,
naam, viko saba vilivyo chukizo kwake:
17 [g]macho ya kiburi,
ulimi udanganyao,
mikono imwagayo damu isiyo na hatia,
18 [h]moyo uwazao mipango miovu,
miguu iliyo myepesi kukimbilia uovu,
19 [i]shahidi wa uongo ambaye humwaga uongo,
na mtu ambaye huchochea fitina kati ya ndugu.

*Onyo Dhidi Ya Uasherati*

20 [j]Mwanangu, zishike amri za baba yako,
wala usiyaache mafundisho ya mama yako.
21 [k]Yafunge katika moyo wako daima,
yakaze kuizunguka shingo yako.
22 [l]Wakati utembeapo, yatakuongoza;
wakati ulalapo, yatakulinda;
wakati uamkapo, yatazungumza nawe.
23 [m]Kwa maana amri hizi ni taa,
mafundisho haya ni mwanga
na maonyo ya maadili ni njia ya uzima,
24 [n]yakikulinda na mwanamke aliyepotoka,
kutokana na maneno laini ya mwanamke aliyepotoka.
25 [o]Moyo wako usitamani uzuri wake
wala macho yake yasikuteke,

---

[a]**6:9** Mit 24:30-34; 26:13-16
[b]**6:10** Mit 24:33; Mhu 4:5
[c]**6:11** Mit 6:10-11; 20:13; 24:30-34
[d]**6:13** Za 35:19; Mit 16:30
[e]**6:14** Za 36:4; 140:2; Mik 2:1; Isa 32:7
[f]**6:16** Mit 3:32; 8:13; 15:8, 9, 26; 16:5
[g]**6:17** Za 120:2; Mit 12:22; Yer 2:34; Mik 7:2; Hos 4:1-2
[h]**6:18** Mwa 6:5; Ay 15:31; Rum 3:15
[i]**6:19** Kum 19:16; Za 27:12; Mit 15:18; Zek 8:17
[j]**6:20** Mit 3:21; 1:8
[k]**6:21** Kum 6:8; Mit 3:3
[l]**6:22** Mit 3:23; 2:11
[m]**6:23** Za 19:8; 10:17
[n]**6:24** Mwa 39:8; Za 55:21
[o]**6:25** 2Sam 11:2-5; Mt 5:28

26 [a]kwa maana kahaba atakufanya uwe
maskini,
hata ukose kipande cha mkate,
naye mwanamke mzinzi huwinda
maisha yako hasa.
27 Je, mtu aweza kuchotea moto
kwenye paja lake
bila nguo zake kuungua?
28 Je, mtu aweza kutembea juu ya
makaa ya moto yanayowaka
bila miguu yake kuungua?
29 [b]Ndivyo alivyo mtu alalaye na mke
wa mwanaume mwingine;
hakuna yeyote amgusaye
huyo mwanamke ambaye
hataadhibiwa.

30 Watu hawamdharau mwizi kama
akiiba
kukidhi njaa yake wakati ana njaa.
31 [c]Pamoja na hayo, kama akikamatwa,
lazima alipe mara saba,
ingawa inamgharimu utajiri wote
wa nyumba yake.
32 [d]Lakini mwanaume aziniye na
mwanamke hana akili kabisa;
yeyote afanyaye hivyo
hujiangamiza mwenyewe.
33 [e]Mapigo na aibu ni fungu lake
na aibu yake haitafutika kamwe;
34 [f]kwa maana wivu huamsha
ghadhabu ya mume,
naye hataonyesha huruma
alipizapo kisasi.
35 [g]Hatakubali fidia yoyote;
atakataa malipo, hata yakiwa
makubwa kiasi gani.

*Onyo Dhidi Ya Mwanamke Mzinzi*

7 [h]Mwanangu, shika maneno yangu
na kuzihifadhi amri zangu
ndani yako.
2 [i]Shika amri zangu nawe utaishi;
linda mafundisho yangu kama
mboni ya jicho lako.
3 [j]Yafunge katika vidole vyako;
yaandike katika kibao cha moyo
wako.
4 Mwambie hekima, “Wewe ni dada
yangu,”
uite ufahamu jamaa yako;
5 [k]watakuepusha na mwanamke
mzinzi,
kutokana na mwanamke mpotovu
na maneno yake ya kubembeleza.

6 Kwenye dirisha la nyumba yangu
nilitazama nje kupitia upenyo
kwenye mwimo wa dirisha.
7 [l]Niliona miongoni mwa wajinga,
nikagundua miongoni mwa
wanaume vijana,
kijana asiye na akili.
8 Alikuwa akishuka njiani karibu na
pembe ya kwake,
akielekea kwenye nyumba ya huyo
mwanamke
9 [m]wakati wa machweo, jua likipungua
nuru yake,
giza la usiku lilipokuwa likiingia.

10 [n]Ndipo huyo mwanamke akatoka
kumlaki,
hali amevaa kama kahaba akiwa
na nia ya udanganyifu.
11 [o](Ni mwanamke mwenye makelele
na mkaidi,
miguu yake haitulii nyumbani;
12 [p]mara kwenye barabara za mji,
mara kwenye viwanja vikubwa,
kwenye kila pembe huvizia.)

[a]**6:26** Mit 27:22-23; 29:3; Eze 13:18
[b]**6:29** Kut 20:14; Mit 2:16-19
[c]**6:31** Kut 22:1-14
[d]**6:32** Kut 20:14; Mit 7:7; 9:4, 16
[e]**6:33** Mit 5:9-14
[f]**6:34** Hes 5:14; Mwa 34:7
[g]**6:35** Ay 31:9-11; Wim 8:7
[h]**7:1** Mt 1:8
[i]**7:2** Mit 4:4; Law 18:5; Kum 32:10
[j]**7:3** Kum 6:8; Mit 3:3; Isa 30:8; 2Kor 3:3
[k]**7:5** Ay 31:9; Mit 2:16
[l]**7:7** Mit 6:32
[m]**7:9** Ay 24:15
[n]**7:10** 1Tim 2:9
[o]**7:11** Mit 9:13; 1Tim 5:13
[p]**7:12** Mit 8:1-36; 23:26-28

13 [a]Huyo mwanamke alimkumbatia
kijana na kumbusu,
na kwa uso usio na haya
akamwambia:

14 [b]"Nina sadaka za amani nyumbani;
leo nimetimiza nadhiri zangu.
15 Kwa hiyo nimetoka nje kukulaki;
nimekutafuta na nimekupata!
16 [c]Nimetandika kitanda changu
kwa kitani za rangi kutoka Misri.
17 [d]Nimetia manukato kitanda changu
kwa manemane, udi na mdalasini.
18 [e]Njoo, tuzame katika mapenzi mpaka
asubuhi;
tujifurahishe wenyewe kwa
mapenzi!
19 Mume wangu hayupo nyumbani;
amekwenda safari ya mbali.
20 Amechukua mkoba uliojazwa fedha
na hatakuwepo nyumbani
karibuni."

21 [f]Kwa maneno laini yule mwanamke
akampotosha;
alimshawishi kwa maneno yake
laini.
22 [g]Mara huyo kijana alimfuata yule
mwanamke
kama fahali aendaye machinjoni,
kama kulungu aingiaye kwenye
kitanzi,
23 [h]mpaka mshale umchome ini lake,
kama ndege anayenaswa kwenye
mtego,
bila kujua itamgharimu maisha
yake.

24 [i]Sasa basi wanangu, nisikilizeni;
sikilizeni kwa makini nisemalo.
25 [j]Usiruhusu moyo wako ugeukie njia
za huyo mwanamke,
wala usitangetange katika mapito
yake.
26 [k]Aliowaangusha ni wengi;
aliowachinja ni kundi kubwa.
27 [l]Nyumba yake ni njia kuu iendayo
kaburini,[m]
ielekeayo chini kwenye vyumba
vya mauti.

*Wito Wa Hekima*

8 [n]Je, hekima haitani?
Je, ufahamu hapazi sauti?
2 Juu ya miinuko karibu na njia,
penye njia panda, ndipo
asimamapo;
3 [o]kando ya malango yaelekeayo mjini,
kwenye maingilio, hulia kwa sauti
kubwa, akisema:
4 [p]"Ni ninyi wanaume, ninaowaita;
ninapaza sauti yangu kwa
wanadamu wote.
5 [q]Ninyi ambao ni wajinga, pateni
akili;
ninyi mlio wapumbavu, pateni
ufahamu.
6 [r]Sikilizeni, kwa maana nina mambo
muhimu ya kusema;
ninafungua midomo yangu
kusema lililo sawa.
7 [s]Kinywa changu husema lililo kweli,
kwa maana midomo yangu
huchukia uovu.
8 Maneno yote ya kinywa changu ni
haki;
hakuna mojawapo lililopotoka
wala ukaidi.

---

[a]**7:13** Mwa 39:12; Mit 1:20
[b]**7:14** Law 7:11-18
[c]**7:16** Isa 19:9
[d]**7:17** Amo 6:4; Mwa 37:25
[e]**7:18** Mwa 39:7
[f]**7:21** Mit 1:8-9; 8:32
[g]**7:22** Ay 18:10
[h]**7:23** Ay 15:22; 16:13; Mit 6:26; Mhu 9:12
[i]**7:24** Mit 1:8-9; 8:32
[j]**7:25** Mit 5:7-8
[k]**7:26** Neh 13:26
[l]**7:27** Amu 16:19; Ufu 22:15
[m]27 Kaburini hapa maana yake ni Kuzimu, kwa Kiebrania ni Sheol.
[n]**8:1** Mit 1:20; 9:3; Ay 28:12; 1Kor 1:24
[o]**8:3** Ay 29:7; Mit 7:6-13
[p]**8:4** Isa 42:2
[q]**8:5** Mit 1:22; 1:4
[r]**8:6** Za 49:3; Mt 2:6, 7; Kol 1:26
[s]**8:7** Za 37:30; Yn 8:14; Rum 15:8

9 Kwa wenye kupambanua yote ni sahihi;
hayana kasoro kwa wale wenye maarifa.
10 [a]Chagua mafundisho yangu badala ya fedha,
maarifa badala ya dhahabu safi,
11 [b]kwa maana hekima ina thamani kuliko marijani
na hakuna chochote unachohitaji kinacholingana naye.

12 [c]"Mimi hekima, nakaa pamoja na busara;
ninamiliki maarifa na busara.
13 [d]Kumcha BWANA ni kuchukia uovu;
ninachukia kiburi na majivuno,
tabia mbaya na mazungumzo potovu.
14 [e]Ushauri na hukumu sahihi ni vyangu;
nina ufahamu na nina nguvu.
15 [f]Kwa msaada wangu wafalme hutawala
na watawala hutunga sheria zilizo za haki,
16 [g]kwa msaada wangu wakuu hutawala,
na wenye vyeo wote watawalao dunia.
17 [h]Nawapenda wale wanipendao,
na wale wanitafutao kwa bidii wataniona.
18 [i]Utajiri na heshima viko kwangu,
utajiri udumuo na mafanikio.
19 [j]Tunda langu ni bora kuliko dhahabu safi;
kile nitoacho hupita fedha iliyo bora.
20 Natembea katika njia ya unyofu
katika mapito ya haki,
21 [k]nawapa utajiri wale wanipendao
na kuzijaza hazina zao.

22 [l]"BWANA aliniumba mwanzoni mwa kazi yake,
kabla ya matendo yake ya zamani;
23 [m]niliteuliwa tangu milele,
tangu mwanzoni, kabla ya dunia kuumbwa.
24 [n]Wakati hazijakuwepo bahari, nilikwishazaliwa,
wakati hazijakuwepo chemchemi zilizojaa maji;
25 [o]kabla milima haijawekwa mahali pake,
kabla vilima havijakuwepo, nilikwishazaliwa,
26 [p]kabla hajaumba dunia wala mashamba yake
au vumbi lolote la dunia.
27 [q]Nilikuwepo alipoziweka mbingu mahali pake,
wakati alichora mstari wa upeo wa macho
juu ya uso wa kilindi,
28 [r]wakati aliweka mawingu juu
na kuziweka imara chemchemi za bahari,
29 [s]wakati aliiwekea bahari mpaka wake
ili maji yasivunje agizo lake,
na wakati aliweka misingi ya dunia.
30 Wakati huo nilikuwa fundi stadi kando yake.
Nilijazwa na furaha siku baada ya siku,
nikifurahi daima mbele zake,
31 [t]nikifurahi katika dunia yake yote
nami nikiwafurahia wanadamu.

[a]**8:10** Za 19:10; Mit 3:14-15
[b]**8:11** Ay 28:15-19; Mit 3:13-15
[c]**8:12** Mit 1:4
[d]**8:13** Kut 20:20; Yer 44:4; Zek 8:17; Mit 16:6
[e]**8:14** Mhu 7:19; Ay 9:4
[f]**8:15** Dan 2:21; Mt 28:18; Rum 13:1
[g]**8:16** 2Nya 1:10; Mit 29:4
[h]**8:17** Za 91:14; Yn 14:21-24; 1Sam 2:30; Yak 1:5
[i]**8:18** Mt 6:33; 1Fal 3:13; Kum 8:18; Mit 3:16
[j]**8:19** Mit 3:13-14; 10:20
[k]**8:21** Mit 15:6; 24:4
[l]**8:22** Mit 3:19; Yn 1:1
[m]**8:23** Mwa 1:26; Za 2:6; Mik 5:2; Yn 17:24
[n]**8:24** Mwa 7:11
[o]**8:25** Ay 15:7
[p]**8:26** Za 90:2
[q]**8:27** Ay 26:7; Mit 3:19
[r]**8:28** Ay 36:29; Mwa 1:7; Ay 9:8; 26:10
[s]**8:29** Ay 38:8-10; 1Sam 2:8
[t]**8:31** Ay 28:25-27; Yn 1:1-4

32 [a]“Basi sasa wanangu, nisikilizeni;
heri wale wanaozishika njia zangu.
33 Sikilizeni mafundisho yangu mwe na hekima;
msiyapuuze.
34 [b]Heri mtu yule anisikilizaye mimi,
akisubiri siku zote malangoni mwangu,
akingoja kwenye vizingiti vya mlango wangu.
35 [c]Kwa maana yeyote anipataye mimi amepata uzima
na kujipatia kibali kutoka kwa Bwana.
36 [d]Lakini yeyote ashindwaye kunipata hujiumiza mwenyewe;
na wote wanichukiao mimi hupenda mauti.”

*Makaribisho Ya Hekima Na Ya Upumbavu*

9 [e]Hekima amejenga nyumba yake;
amechonga nguzo zake saba.
2 [f]Ameandaa nyama na kuchanganya divai yake;
pia ameandaa meza yake.
3 [g]Amewatuma watumishi wake wa kike, naye huita
kutoka mahali pa juu sana pa mji.
4 [h]Anawaambia wale wasio na akili,
“Wote ambao ni wajinga na waje hapa!
5 [i]Njooni, mle chakula changu
na mnywe divai niliyoichanganya.
6 [j]Acheni njia zenu za ujinga nanyi mtaishi;
tembeeni katika njia ya ufahamu.

7 [k]“Yeyote anayemkosoa mwenye mzaha
hukaribisha matukano;
yeyote anayekemea mtu mwovu
hupatwa na matusi.
8 Usimkemee mwenye mzaha la sivyo atakuchukia;
mkemee mwenye hekima naye atakupenda.
9 [l]Mfundishe mtu mwenye hekima
naye atakuwa na hekima zaidi;
mfundishe mtu mwadilifu
naye atazidi kufundishika.

10 [m]“Kumcha Bwana ndicho chanzo cha hekima,
na kumjua Aliye Mtakatifu ni ufahamu.
11 [n]Kwa maana kwa msaada wangu
siku zako zitakuwa nyingi,
na miaka itaongezwa katika maisha yako.
12 [o]Kama wewe una hekima, hekima yako itakupa tuzo;
kama wewe ni mtu wa mzaha,
wewe mwenyewe ndiwe utateseka.”

13 [p]Mwanamke aitwaye Mpumbavu ana kelele;
hana adabu na hana maarifa.
14 [q]Huketi kwenye mlango wa nyumba yake,
juu ya kiti katika mahali pa juu sana pa mji,
15 [r]akiita wale wapitao karibu,
waendao moja kwa moja kwenye njia yao.
16 [s]Anawaambia wale wasio na akili,
“Wote ambao ni wajinga na waje hapa ndani!”

[a]**8:32** Lk 11:28; 2Sam 22:22; Za 119:1-2
[b]**8:34** 1Fal 10:8; Mit 3:13-18; Flp 3:8-9
[c]**8:35** Yn 3:16, 36; Flp 3:8, 9; Mit 13:18; 9:6; Yn 5:39-40
[d]**8:36** Isa 3:9; Yer 40:2
[e]**9:1** Efe 2:20-22; 1Tim 3:15; 1Pet 3:5
[f]**9:2** Lk 14:16-23; Isa 25:6; 62:8
[g]**9:3** Mit 1:20; 8:1-3; Mt 22:3, 4, 9; Lk 14:17; Rum 10:15
[h]**9:4** Mit 1:22; 6:32; Mt 11:25
[i]**9:5** Za 42:2; Isa 44:3; Mt 26:26-28
[j]**9:6** Mit 8:35; 3:1-2
[k]**9:7** Mit 23:9; Mt 7:6
[l]**9:9** Mit 15:31; 19:25; Mt 13:12
[m]**9:10** Ay 28:28
[n]**9:11** Mwa 15:15; Kum 11:21; Mit 10:27
[o]**9:12** Ay 35:6, 7
[p]**9:13** Mit 7:11; 5:6
[q]**9:14** Eze 16:25
[r]**9:15** Mit 1:20
[s]**9:16** Mit 1:22

17 [a]"Maji yaliyoibiwa ni matamu;
chakula kinacholiwa sirini ni
kitamu!"
18 [b]Lakini hawajui hata kidogo kuwa
wafu wako humo,
kwamba wageni wake huyo
mwanamke
wako katika vilindi vya kuzimu.

*Mithali Za Solomoni*

10 [c]Mithali za Solomoni:

Mwana mwenye
hekima
huleta furaha kwa baba yake,
lakini mwana mpumbavu
huleta huzuni kwa mama yake.

2 [d]Hazina zilizopatikana kwa njia
mbaya hazifai,
lakini uadilifu huokoa kutoka
mautini.

3 [e]BWANA hawaachi waadilifu kukaa
njaa,
lakini hupinga tamaa ya mtu
mwovu.

4 [f]Mikono mivivu hufanya mtu kuwa
maskini
lakini mikono yenye bidii huleta
utajiri.

5 [g]Yeye akusanyaye mazao wakati wa
kiangazi
ni mwana mwenye hekima,
lakini yeye alalaye wakati wa
mavuno
ni mwana mwenye kuaibisha.

6 [h]Baraka huwa taji kichwani mwa
mwenye haki,
lakini jeuri hufunika kinywa cha
mwovu.

7 [i]Kumbukumbu ya mwenye haki
itakuwa baraka,
lakini jina la mwovu litaoza.

8 [j]Mwenye hekima moyoni hupokea
maagizo,
lakini mpumbavu apayukaye
huangamia.

9 [k]Mtu mwadilifu hutembea salama,
lakini mtu aendaye katika njia
zilizopotoka atagunduliwa.

10 [l]Yeye akonyezaye kwa nia mbaya
husababisha huzuni,
naye mpumbavu apayukaye
huangamia.

11 [m]Kinywa cha mwenye haki ni
chemchemi ya uzima,
lakini jeuri hufunika kinywa cha
mwovu.

12 [n]Chuki huchochea faraka,
lakini upendo husitiri mabaya
yote.

13 [o]Hekima hupatikana katika midomo
ya wenye kupambanua,
lakini fimbo ni kwa ajili ya
mgongo wake asiye na
ufahamu.

14 [p]Wenye hekima huhifadhi maarifa,
bali kinywa cha mpumbavu
hualika maangamizi.

15 [q]Mali ya tajiri ni mji wake wenye
ngome,
bali ufukara ni maangamizi ya
maskini.

---

[a]**9:17** Mit 20:17
[b]**9:18** Mit 2:18; 7:26-27
[c]**10:1** 1Fal 4:32; Mit 1:1; 15:20; 17:21; 19:13; 23:22; 27:11; 29:3
[d]**10:2** Dan 4:27; Mit 13:11; 21:6; 12:28; Lk 12:29
[e]**10:3** Za 10:14; Mt 6:25-34
[f]**10:4** Mit 24:30-34; 13:4
[g]**10:5** Mit 24:30-34
[h]**10:6** Es 7:8; Mit 13:3; Mhu 10:12
[i]**10:7** Mhu 8:10; Ay 18:17; Za 109:13
[j]**10:8** Ay 33:33; Mt 7:24-27
[k]**10:9** Za 23:4; 25:21; Isa 33:15; Mit 28:18
[l]**10:10** Za 35:19
[m]**10:11** Za 37:30; Mit 3:18
[n]**10:12** Mit 17:9; 1Kor 13:4-7; 1Pet 4:8
[o]**10:13** Za 37:30; Mit 15:7; Kum 25:2; Lk 4:22
[p]**10:14** Za 59:12; Mt 12:37
[q]**10:15** Mit 18:11; Ay 31:24; 1Tim 6:17

16 [a]Ujira wa wenye haki huwaletea uzima,
lakini mapato ya waovu huwaletea adhabu.

17 [b]Anayekubali kuadibishwa yuko katika njia ya uzima,
lakini yeyote anayepuuza maonyo hupotosha wengine.

18 [c]Yeye afichaye chuki yake ana midomo ya uongo,
na yeyote anayeeneza uchonganishi ni mpumbavu.

19 [d]Wakati maneno ni mengi, dhambi haikosekani,
lakini yeye ambaye huzuia ulimi wake ni mwenye busara.

20 Ulimi wa mwenye haki ni fedha iliyo bora,
bali moyo wa mwovu una thamani ndogo.

21 [e]Midomo ya mwenye haki hulisha wengi,
lakini wapumbavu hufa kwa kukosa ufahamu.

22 [f]Baraka ya BWANA hutajirisha,
wala haichanganyi huzuni.

23 [g]Mpumbavu hufurahia tabia mbaya,
lakini mtu mwenye ufahamu hupendezwa na hekima.

24 [h]Kile anachoogopa mwovu ndicho kitakachompata;
kile anachoonea shauku mwenye haki atapewa.

25 [i]Tufani inapopita, waovu hutoweka,
lakini wenye haki husimama imara milele.

26 [j]Kama siki ilivyo kwa meno na moshi kwa macho,
ndivyo alivyo mvivu kwa wale waliomtuma.

27 [k]Kumcha BWANA huongeza urefu wa maisha,
lakini miaka ya mwovu inafupishwa.

28 [l]Tarajio la mwenye haki ni furaha,
bali matumaini ya mwovu huwa si kitu.

29 [m]Njia ya BWANA ni kimbilio kwa wenye haki,
lakini ni maangamizi ya wale watendao mabaya.

30 [n]Kamwe wenye haki hawataondolewa,
bali waovu hawatasalia katika nchi.

31 [o]Kinywa cha mwenye haki hutoa hekima,
bali ulimi wa upotovu utakatwa.

32 [p]Midomo ya wenye haki inajua kile kinachofaa,
bali kinywa cha mwovu hujua kile kilichopotoka tu.

11 [q]BWANA huchukia sana mizani za udanganyifu,
bali vipimo sahihi ni furaha yake.

2 [r]Kiburi kinapokuja, ndipo huja aibu,
bali unyenyekevu huja na hekima.

3 [s]Uadilifu wa wenye haki huwaongoza,
bali wasio waaminifu huharibiwa na hila yao.

---

[a]**10:16** Kum 30:15; Mit 11:18-19; 15:6; Rum 6:23
[b]**10:17** Mit 6:23; 15:5
[c]**10:18** Za 31:18
[d]**10:19** Yak 1:19; Mhu 5:3; Za 39:1
[e]**10:21** Isa 5:13; Yer 5:4
[f]**10:22** Mwa 12:2; 13:2; Za 37:22; Kum 8:17-18
[g]**10:23** Mit 2:14
[h]**10:24** Isa 66:4; Mt 5:6; Ay 15:21
[i]**10:25** Za 20:8; Mt 7:24-27
[j]**10:26** Isa 65:5; Mit 13:17; 25:13; 26:6
[k]**10:27** Kum 11:9; Mit 22:4; Mhu 7:17; Ay 15:32
[l]**10:28** Es 7:10; Ay 8:13; Za 16:9
[m]**10:29** Za 10:12; Mit 21:15; Hos 14:9
[n]**10:30** Za 37:28-29; Mit 2:20-22
[o]**10:31** Mit 10:13; 15:2; 31:26; Za 52:4
[p]**10:32** Mhu 10:12; Za 59:7
[q]**11:1** Law 19:36; Ay 6:2; Mit 16:11; Eze 45:10
[r]**11:2** Dan 4:30; Mit 16:18; 18:12
[s]**11:3** Mit 13:6

4 [a]Utajiri haufaidi kitu katika siku ya ghadhabu,
bali haki huokoa kutoka mautini.

5 [b]Haki ya wasio na lawama, huwatengenezea njia iliyonyooka,
bali waovu huangushwa kwa uovu wao wenyewe.

6 [c]Haki ya wanyofu huwaokoa,
bali wasio waaminifu hunaswa na tamaa mbaya.

7 [d]Wakati mtu mwovu anapokufa, matumaini yake hutoweka;
yote aliyoyatazamia kutokana na nguvu zake huwa si kitu.

8 [e]Mtu mwenye haki huokolewa kutoka taabu,
naye mtu mwovu huingia humo badala yake.

9 [f]Kwa kinywa chake mtu asiyemwamini Mungu
humwangamiza jirani yake,
bali kwa maarifa mwenye haki huokolewa.

10 [g]Wakati mwenye haki anapofanikiwa, mji hufurahi;
mwovu atowekapo, kuna kelele za furaha.

11 [h]Kutokana na baraka ya mtu mnyofu mji hukwezwa,
bali kwa kinywa cha mwovu mji huharibiwa.

12 [i]Mtu asiye na akili humdharau jirani yake,
bali mtu mwenye ufahamu huuzuia ulimi wake.

13 [j]Masengenyo husaliti tumaini,
bali mtu mwaminifu hutunza siri.

14 [k]Pasipo ushauri wa hekima taifa huanguka,
bali washauri wengi hufanya ushindi uwe wa hakika.

15 [l]Yeye amdhaminiye mgeni hakika atateseka,
bali yeyote akataaye kuunga mkono dhamana ni salama.

16 [m]Mwanamke mwenye moyo wa huruma hupata heshima,
bali wanaume wakorofi hupata mali tu.

17 [n]Mwenye huruma hujinufaisha mwenyewe,
bali mkatili hujiletea taabu mwenyewe.

18 [o]Mtu mwovu hupata ujira wa udanganyifu,
bali yeye apandaye haki huvuna tuzo ya uhakika.

19 [p]Mtu mwenye haki kweli kweli hupata uzima,
bali yeye afuatiliaye ubaya huendea kifo chake.

20 [q]Bwana huwachukia sana watu wenye moyo wa upotovu,
bali hupendezwa na wale ambao njia zao hazina lawama.

21 [r]Uwe na hakika na hili: Waovu hawataepuka kuadhibiwa,
bali wenye haki watakuwa huru.

---

[a]**11:4** Ay 20:20; Eze 7:19; Sef 1:18
[b]**11:5** 1Fal 8:36; Mit 5:21-23; 13:6; 21:7
[c]**11:6** Es 7:9; 1Tim 4:8; Mhu 10:8
[d]**11:7** Ay 8:13; Mit 10:28
[e]**11:8** Mit 21:8
[f]**11:9** Mit 12:6; Yer 45:5; Ay 8:13
[g]**11:10** 2Fal 11:20; Mit 28:12; Es 8:15
[h]**11:11** Mit 14:34; 29:8
[i]**11:12** Mit 14:21; Ay 6:24
[j]**11:13** Law 19:16; 1Tim 5:13; Mit 20:19; 10:14
[k]**11:14** Mit 20:18; 24:6; 2Sam 15:34; 1Fal 12:1; Mit 20:18; 2Sam 15:34; Mit 15:22; 24:6; 1Fal 12:1
[l]**11:15** Mit 6:1; 17:18; 22:26-27
[m]**11:16** Mit 31:31
[n]**11:17** Mt 25:34
[o]**11:18** Hos 10:12; Kut 1:20; Ay 4:8
[p]**11:19** Kum 30:15; Mit 10:2; 1Sam 2:6; Za 89:48; Mit 1:18-19; Mhu 7:2; Yer 43:1
[q]**11:20** 1Nya 29:17; Za 52:7
[r]**11:21** Mit 16:5; Za 112:2

22 Kama pete ya dhahabu katika pua ya nguruwe
ndivyo alivyo mwanamke mzuri ambaye hana busara.

23 [a]Shauku ya mwenye haki huishia tu kwenye mema,
bali tumaini la mwovu huishia tu kwenye ghadhabu.

24 [b]Kuna mtu atoaye kwa ukarimu, hata hivyo hupata zaidi,
mwingine huzuia, lakini huwa maskini.

25 [c]Mtu mkarimu atastawi;
yeye awaburudishaye wengine ataburudishwa mwenyewe.

26 [d]Watu humlaani mtu awanyimae watu nafaka,
bali baraka itamkalia kichwani kama taji
yeye aliye radhi kuiuza.

27 [e]Yeye atafutaye mema hupata ukarimu,
bali ubaya huja kwake yeye autafutaye.

28 [f]Yeyote ategemeaye utajiri wake ataanguka,
bali mwenye haki atastawi kama jani bichi.

29 [g]Yeye aletaye taabu kwa jamaa yake atarithi tu upepo,
naye mpumbavu atakuwa mtumishi wa wenye hekima.

30 [h]Tunda la mwenye haki ni mti wa uzima,
naye mwenye hekima huvuta roho za watu.

31 [i]Kama wenye haki watapokea ujira wao duniani,
si zaidi sana yule asiyemcha Mungu na mwenye dhambi?

*Mafundisho Ya Kifamilia Na Ya Kijamii*

12 [j]Yeyote apendaye kuadibishwa hupenda maarifa,
bali yeye achukiaye kuonywa ni mpumbavu.

2 [k]Mtu mwema hupata kibali kutoka kwa BWANA,
bali BWANA humhukumu mwenye hila.

3 [l]Mtu hathibitiki kutokana na uovu,
bali mwenye haki hataondolewa.

4 [m]Mke mwenye tabia nzuri ni taji ya mumewe,
bali aaibishaye ni kama uozo
katika mifupa ya mumewe.

5 Mipango ya mtu mwadilifu ni ya haki,
bali ushauri wa mwovu ni udanganyifu.

6 [n]Maneno ya waovu huotea kumwaga damu,
bali maneno ya waadilifu huwaokoa.

7 [o]Watu waovu huondolewa na kutoweka,
bali nyumba ya mwenye haki husimama imara.

8 [p]Mtu husifiwa kulingana na hekima yake,
bali watu wenye akili zilizopotoka hudharauliwa.

---

[a]**11:23** Rum 2:8, 9
[b]**11:24** Za 112:9
[c]**11:25** Mit 22:9; 2Kor 9:6-9; Mt 5:7
[d]**11:26** Amo 8:5; Ay 29:13
[e]**11:27** Es 7:10; Za 7:15-16
[f]**11:28** Yer 9:23; 17:8; Mk 10:25; Za 52:8
[g]**11:29** Mhu 5:16; Mit 14:19
[h]**11:30** Mwa 2:9; Yak 5:20
[i]**11:31** Yer 25:29; 49:12; 1Pet 4:18
[j]**12:1** Mit 5:11-14; 9:7-9; 13:1, 18; 15:5, 10
[k]**12:2** Ay 33:26; Za 84:11; 2Sam 15:3; Mit 11:20
[l]**12:3** Mit 10:25
[m]**12:4** Mit 14:30; 31:23; 1Kor 11:7; Rum 3:11
[n]**12:6** Mit 11:9; 14:3
[o]**12:7** Mt 7:24; Za 37:34; Mit 14:11; 15:25
[p]**12:8** 1Sam 13:13; Mal 2:8-9; Mt 27:4-5

9 Heri mtu wa hali ya chini mwenye
mtumishi,
kuliko kujifanya mtu wa hali ya
juu nawe huna chakula.

10 [a]Mtu mwenye haki hujali mahitaji ya
mnyama wake,
bali matendo ya huruma ya
mwovu ni ukatili.

11 [b]Yeye alimaye shamba lake atakuwa
na chakula tele,
bali yeye afuataye mambo ya
upuzi hana akili.

12 [c]Waovu hutamani mateka ya watu
wabaya,
bali shina la mwenye haki
hustawi.

13 [d]Mtu mwovu hunaswa kwa
mazungumzo yake ya dhambi,
bali mwenye haki huepuka taabu.

14 [e]Kutokana na tunda la midomo yake
mtu hujazwa na mambo mema,
hakika kama ilivyo kazi ya mikono
yake humtunza.

15 [f]Njia ya mpumbavu huonekana sawa
machoni pake mwenyewe,
bali mtu mwenye hekima
husikiliza ushauri.

16 [g]Mpumbavu huonyesha kuudhika
kwake mara moja,
bali mtu wa busara hupuuza
matukano.

17 [h]Shahidi wa kweli hutoa ushuhuda
wa kuaminika,
bali shahidi wa uongo husema
uongo.

18 [i]Maneno ya kipumbavu huchoma
kama upanga,
bali ulimi wa mwenye hekima
huleta uponyaji.

19 [j]Midomo isemayo kweli hudumu
milele,
bali ulimi wa uongo hudumu kwa
muda mfupi tu.

20 [k]Upo udanganyifu katika mioyo
ya wale ambao hupanga mabaya,
bali kuna furaha kwa wale
wanaoleta amani.

21 [l]Hakuna dhara linalompata mwenye
haki,
bali waovu wana taabu nyingi.

22 [m]Bwana anachukia sana midomo
idanganyayo,
bali hufurahia watu ambao ni wa
kweli.

23 [n]Mtu mwenye busara hujihifadhia
maarifa yeye mwenyewe,
bali moyo wa wapumbavu
hububujika upumbavu.

24 [o]Mikono yenye bidii itatawala,
bali uvivu huishia katika kazi za
utumwa.

25 [p]Moyo wa wasiwasi humlemea mtu,
bali neno la huruma
humfurahisha.

26 [q]Mtu mwenye haki ni mwangalifu
katika urafiki,
bali njia ya waovu huwapotosha.

27 Mtu mvivu haoki mawindo yake,
bali mtu mwenye bidii ana mali za
thamani.

[a]**12:10** Kum 25:4; Hes 22:29
[b]**12:11** Mwa 3:19; Efe 4:28
[c]**12:12** Za 1:3; Lk 8:15
[d]**12:13** Za 59:12; Mit 10:6; 21:23; 2Pet 2:9
[e]**12:14** Mit 15:23; 14:14; Isa 3:10-11
[f]**12:15** Mit 16:2, 25; Lk 18:11
[g]**12:16** 1Sam 25:25; Ay 5:2; Mit 29:11
[h]**12:17** Za 12:2; Mit 14:5, 25
[i]**12:18** Za 57:4; Mit 25:18; 15:4
[j]**12:19** Zek 1:5, 6
[k]**12:20** Rum 14:19
[l]**12:21** Ay 4:7; Za 91:10; Rum 8:28
[m]**12:22** 1Fal 13:18; Ufu 22:15; Mit 11:20
[n]**12:23** Mit 10:14; Za 38:5; 59:7; Mit 18:2
[o]**12:24** Mit 10:4; 1Fal 11:28
[p]**12:25** Mit 15:13; Isa 50:4
[q]**12:26** Za 95:10

28 [a]Katika njia ya haki kuna uzima;
katika mapito hayo kuna maisha
ya milele.

*Mema Ya Muda Mfupi Na Yale Ya Kudumu*

13 [b]Mwana mwenye hekima husikia
mafundisho ya babaye,
bali mwenye dharau hasikilizi
maonyo.

2 [c]Kutoka tunda la midomo yake mtu
hufurahia mambo mema,
bali wasio waaminifu wanatamani
sana jeuri.

3 [d]Yeye alindaye midomo yake
hulinda nafsi yake,
bali yeye asemaye kwa haraka
ataangamia.

4 [e]Mvivu hutamani sana na hapati
kitu,
bali nafsi ya mwenye bidii
hutoshelezwa kikamilifu.

5 [f]Mwenye haki huchukia uongo,
bali waovu huleta aibu na
fedheha.

6 [g]Haki humlinda mtu mwadilifu,
bali uovu humwangusha mwenye
dhambi.

7 [h]Mtu mmoja hujifanya tajiri, kumbe
hana chochote;
mwingine hujifanya maskini, kumbe
ana utajiri mwingi.

8 [i]Utajiri wa mtu waweza kukomboa
maisha yake,
bali mtu maskini hasikii kitisho.

9 [j]Nuru ya mwenye haki hung'aa sana,
bali taa ya mwovu itazimwa.

10 [k]Kiburi huzalisha magomvi tu,
bali hekima hupatikana kwa wale
wanaozingatia ushauri.

11 [l]Fedha isiyo ya halali hupungua,
bali yeye akusanyaye fedha kidogo
kidogo huongezeka.

12 [m]Kilichotarajiwa kikikawia kuja
moyo huugua,
bali tumaini lililotimizwa ni mti
wa uzima.

13 [n]Yeye anayedharau mafundisho
anajiletea maangamizi,
bali yeye anayeheshimu agizo
hupewa tuzo.

14 [o]Mafundisho ya mwenye busara ni
chemchemi ya uzima,
ili kumwepusha mtu na mitego ya
mauti.

15 Ufahamu mzuri hupata upendeleo,
bali njia ya asiye mwaminifu ni
ngumu.

16 [p]Kila mwenye busara hutenda kwa
maarifa,
bali mpumbavu hudhihirisha
upumbavu wake.

17 [q]Mjumbe mwovu huanguka kwenye
taabu,
bali mjumbe mwaminifu huleta
uponyaji.

18 [r]Yeye anayedharau maonyo hupata
umaskini na aibu,
bali yeye anayekubali maonyo
huheshimiwa.

---

[a]**12:28** Kum 30:15; Rum 5:21; Mit 10:2
[b]**13:1** 1Sam 2:25; Mit 10:1; 12:1; 15:5
[c]**13:2** Mit 12:14
[d]**13:3** Za 12:2; Yak 3:2; Mit 10:6; Ay 1:22
[e]**13:4** Mit 21:25-26
[f]**13:5** Kol 3:9; Rum 12:9
[g]**13:6** Mit 11:3-5; Yer 44:5
[h]**13:7** 2Kor 6:10
[i]**13:8** Mit 15:16
[j]**13:9** Ay 18:5; Mit 4:18-19
[k]**13:10** Amu 19:30; Mit 9:9
[l]**13:11** Mit 10:2; 9:9; 20:21
[m]**13:12** Mit 10:11
[n]**13:13** Hes 15:31; Kut 9:20; Mit 16:20; 2Nya 36:16
[o]**13:14** Mit 10:11; 14:27
[p]**13:16** Es 5:11; Mit 12:23
[q]**13:17** Mit 10:26; 25:13
[r]**13:18** Mit 15:31-32; Za 141:5

19 [a]Tarajio lililotimizwa ni tamu kwa nafsi,
bali wapumbavu huchukia sana kuacha ubaya.

20 [b]Yeye atembeaye na mwenye hekima atapata hekima,
bali rafiki wa mpumbavu hupata madhara.

21 [c]Balaa humwandama mtenda dhambi,
bali mafanikio ni thawabu kwa mwenye haki.

22 [d]Mtu mwema huwaachia wana wa wanawe urithi,
bali mali ya wenye dhambi imehifadhiwa
kwa ajili ya wenye haki.

23 [e]Shamba la mtu maskini laweza kuzalisha chakula kingi,
bali dhuluma hukifutilia mbali.

24 [f]Yeye aizuiaye fimbo yake hampendi mwanawe,
bali yeye ampendaye
huwa mwangalifu kumwadibisha.

25 [g]Mwenye haki hula mpaka akaridhisha moyo wake,
bali tumbo la mwovu hutaabika kwa njaa.

14 [h]Mwanamke mwenye hekima huijenga nyumba yake,
bali mpumbavu huibomoa nyumba yake
kwa mikono yake mwenyewe.

2 [i]Yeye ambaye njia zake ni nyofu humcha Bwana,
bali yeye ambaye njia zake zimepotoka humdharau Mungu.

3 [j]Mazungumzo ya mpumbavu huleta fimbo mgongoni mwake,
bali mwenye hekima hulindwa na maneno ya midomo yake.

4 [k]Pale ambapo hakuna mafahali, hori ni tupu,
bali kutokana na nguvu za fahali huja mavuno mengi.

5 [l]Shahidi mwaminifu hadanganyi,
bali shahidi wa uongo humimina uongo.

6 [m]Mwenye mzaha huitafuta hekima na haipati,
bali maarifa huja kwa urahisi kwa anayepambanua.

7 Kaa mbali na mtu mpumbavu,
kwa maana hutapata maarifa katika midomo yake.

8 [n]Hekima ya mwenye busara ni kufikiria njia zake,
bali upumbavu wa wapumbavu ni udanganyifu.

9 [o]Wapumbavu hudhihaki kujirekebisha kutoka dhambi,
bali wema hupatikana miongoni mwa wanyofu.

10 Kila moyo hujua uchungu wake wenyewe,
wala hakuna yeyote awezaye kushiriki furaha yake.

11 [p]Nyumba ya mwovu itaangamizwa,
bali hema la mnyofu litastawi.

12 [q]Iko njia ionekanayo kuwa sawa kwa mtu,
bali mwisho wake huelekeza mautini.

---

[a]**13:19** Mit 10:11
[b]**13:20** 2Nya 10:8
[c]**13:21** Za 32:10; Mit 19:17; 11:12
[d]**13:22** Es 8:2; Mhu 2:26
[e]**13:23** Mit 12:11
[f]**13:24** Mit 29:15-17; Efe 6:4
[g]**13:25** Za 34:10; Mit 10:3
[h]**14:1** Rut 3:11; Mit 24:3
[i]**14:2** Ay 12:4
[j]**14:3** Mit 12:6; 10:13
[k]**14:4** Za 12:2; Mit 12:17
[l]**14:5** Kut 20:16; Za 12:2; Mit 6:19
[m]**14:6** Mit 9:9; 17:24
[n]**14:8** Lk 12:20; 1Kor 3:19; Mit 15:28; 21:29
[o]**14:9** Mit 1:22; 10:23
[p]**14:11** Za 72:7; Ay 8:15; Mit 3:33
[q]**14:12** Rum 6:21; Mit 12:15; 16:25

13 [a]Hata katika kicheko moyo waweza kuuma,
nayo furaha yaweza kuishia katika majonzi.

14 [b]Wasio na imani watapatilizwa kikamilifu kwa ajili ya njia zao,
naye mtu mwema atapewa thawabu kwa ajili ya njia yake.

15 [c]Mtu mjinga huamini kila kitu,
bali mwenye busara hufikiria hatua zake.

16 [d]Mtu mwenye hekima humcha BWANA na kuepuka mabaya,
bali mpumbavu hukasirika kwa hamaki na uzembe.

17 [e]Mtu anayekasirika kwa haraka hufanya mambo ya upumbavu,
naye mtu wa hila huchukiwa.

18 Mjinga hurithi upumbavu,
bali wenye busara huvikwa maarifa kichwani kama taji.

19 [f]Watu wabaya watasujudu mbele ya watu wema,
nao waovu kwenye malango ya wenye haki.

20 [g]Maskini huepukwa hata na majirani zao,
bali matajiri wana marafiki wengi.

21 [h]Yeye anayemdharau jirani yake hutenda dhambi,
bali amebarikiwa yeye aliye na huruma kwa mhitaji.

22 [i]Je, wale wanaopanga ubaya hawapotoki?
Bali wale wanaopanga kilicho chema
hupata upendo na uaminifu.

23 Kazi zote zinazofanywa kwa bidii huleta faida,
bali mazungumzo matupu huelekea umaskini tu.

24 [j]Utajiri wa wenye hekima ni taji yao,
bali upumbavu wa wapumbavu huzaa upumbavu.

25 [k]Shahidi wa kweli huokoa maisha,
bali shahidi wa uongo ni mdanganyifu.

26 [l]Yeye amchaye BWANA ana ngome salama,
na kwa watoto wake itakuwa kimbilio.

27 [m]Kumcha BWANA ni chemchemi ya uzima,
ili kumwepusha mtu na mitego ya mauti.

28 [n]Wingi wa watu ni utukufu wa mfalme,
bali pasipo watu mkuu huangamia.

29 [o]Mtu mwenye subira ana ufahamu mwingi,
bali anayekasirika haraka huonyesha upumbavu.

30 [p]Moyo wenye amani huupa mwili uzima,
bali wivu huozesha mifupa.

---

[a]**14:13** Mhu 2:2; 7:3-6
[b]**14:14** 2Nya 15:7; Mit 12:14
[c]**14:15** Mit 14:8
[d]**14:16** Kut 20:20; Mit 22:3
[e]**14:17** Mit 28:25; 29:22
[f]**14:19** Mit 11:29
[g]**14:20** Mit 19:4, 7
[h]**14:21** Mit 11:12; 19:17; Za 41:1
[i]**14:22** Mit 4:16-17
[j]**14:24** Mit 14:8
[k]**14:25** Mit 12:17
[l]**14:26** Mit 19:23; Isa 33:6
[m]**14:27** Za 18:5; Mit 13:14
[n]**14:28** 2Sam 19:7
[o]**14:29** Mhu 7:8-9; Mit 15:18; Yak 1:19
[p]**14:30** Ay 5:2; Mdo 7:9; Mit 12:4

31 [a]Yeye amwoneaye maskini
huonyesha dharau kwa
Muumba wao,
bali yeyote anayemhurumia
mhitaji humheshimu Mungu.

32 [b]Waovu huangamizwa kwa matendo
yao maovu,
bali hata katika kifo wenye haki
hupata kimbilio.

33 [c]Hekima hukaa katika moyo wa
mwenye ufahamu
bali haijulikani miongoni mwa
wapumbavu.

34 [d]Haki huinua taifa,
bali dhambi ni aibu kwa watu
wote.

35 [e]Mfalme hupendezwa na mtumishi
mwenye hekima,
bali ghadhabu yake humwangukia
mtumishi mwenye kuaibisha.

15 [f]Jawabu la upole hugeuza
ghadhabu,
bali neno liumizalo huchochea
hasira.

2 [g]Ulimi wa mwenye hekima husifu
maarifa,
bali kinywa cha mpumbavu
hufoka upumbavu.

3 [h]Macho ya Bwana yako kila mahali,
yakiwaangalia waovu na wema.

4 [i]Ulimi uletao uponyaji ni mti wa
uzima,
bali ulimi udanganyao huponda
roho.

5 Mpumbavu hubeza maonyo ya baba
yake,
bali yeyote akubaliye maonyo
huonyesha busara.

6 [j]Nyumba ya mwenye haki ina hazina
kubwa,
bali mapato ya waovu huwaletea
taabu.

7 [k]Midomo ya mwenye hekima
hueneza maarifa,
bali sivyo ilivyo mioyo ya
wapumbavu.

8 [l]Bwana huchukia sana dhabihu za
waovu,
bali maombi ya wanyofu
humfurahisha Mungu.

9 [m]Bwana huchukia sana njia ya
waovu,
bali huwapenda wale wafuatao
haki.

10 [n]Adhabu kali humngoja yeye aachaye
njia;
yeye achukiaye maonyo atakufa.

11 [o]Mauti[p] na Uharibifu[q] viko wazi
mbele za Bwana:
je, si zaidi sana mioyo ya
wanadamu!

12 Mwenye mzaha huchukia maonyo;
hatataka shauri kwa mwenye
hekima.

13 Moyo wenye furaha hufanya uso
uchangamke,
bali maumivu ya moyoni huponda
roho.

---

[a]**14:31** Ay 31:15-16; Mit 17:5
[b]**14:32** Za 34:21; Mit 6:15; Ay 13:15; 2Tim 4:18
[c]**14:33** Mit 2:6-10
[d]**14:34** Mit 11:11
[e]**14:35** Es 8:2; Mt 25:14-30
[f]**15:1** Mit 25:15; 2Nya 10:7; 1Fal 12:7
[g]**15:2** Mit 12:23; Mhu 10:12; Za 59:7
[h]**15:3** 2Nya 16:9; Ay 34:21; Ebr 4:13; Mit 5:21; Yer 16:17
[i]**15:4** Za 5:9; Mit 10:11; 12:18
[j]**15:6** Mit 8:21; 10:16
[k]**15:7** Mit 15:2; 10:13
[l]**15:8** Isa 61:8; Yer 6:20; Ay 35:13; Yn 9:31; Amo 5:22
[m]**15:9** Kum 7:13; 1Tim 6:11; Isa 51:1-7
[n]**15:10** Mit 15:13; 17:22
[o]**15:11** Ay 26:6; Za 139:8; Isa 2:3; Yn 2:24; Ufu 2:23
[p]11 Yaani Sheol, maana yake ni Kuzimu.
[q]11 Kwa Kiebrania ni Abadon.

14 Moyo wa mwenye ufahamu hutafuta
maarifa,
bali kinywa cha mpumbavu
hujilisha upumbavu.

15 Siku zote za wanaoonewa ni za
taabu,
bali moyo mchangamfu una
karamu ya kudumu.

16 [a]Afadhali kuwa na kidogo pamoja na
kumcha BWANA,
kuliko mali nyingi pamoja na
ghasia.

17 [b]Afadhali chakula cha mboga mahali
palipo na upendo
kuliko nyama ya ndama iliyonona
pamoja na chuki.

18 [c]Mtu mwepesi wa hasira huchochea
ugomvi,
bali mtu mvumilivu hutuliza
ugomvi.

19 [d]Njia ya mvivu imezibwa na miiba,
bali njia ya mwenye haki ni
barabara kuu.

20 [e]Mwana mwenye hekima huleta
furaha kwa baba yake,
bali mtu mpumbavu humdharau
mama yake.

21 [f]Upumbavu humfurahisha mtu
ambaye hana akili,
bali mtu mwenye ufahamu
hushika njia iliyonyooka.

22 [g]Mipango hushindwa kufanikiwa
kwa ajili ya kukosa ushauri,
bali kukiwa na washauri wengi
hufanikiwa.

23 [h]Mtu hupata furaha katika kutoa jibu
linalofaa:
je, ni zuri namna gani neno
lililotoka kwa wakati wake!

24 [i]Mapito ya uzima huelekea juu kwa
ajili ya wenye hekima
kumwepusha asiende chini
kaburini.

25 [j]BWANA hubomoa nyumba ya mtu
mwenye kiburi,
bali huilinda mipaka ya mjane
isiguswe.

26 [k]BWANA huchukia sana mawazo ya
mwovu,
bali mawazo ya wale walio safi
humfurahisha yeye.

27 [l]Mtu mwenye tamaa huletea jamaa
yake taabu,
bali yeye achukiaye rushwa
ataishi.

28 [m]Moyo wa mwenye haki hupima
majibu yake,
bali kinywa cha mwovu hufoka
ubaya.

29 [n]BWANA yuko mbali na waovu,
bali husikia maombi ya wenye
haki.

30 [o]Mtazamo wa tabasamu huleta
furaha moyoni,
nazo habari njema huipa mifupa
afya.

31 [p]Yeye asikilizaye maonyo yatoayo
uzima
atakuwa miongoni mwa wenye
hekima.

---

[a]**15:16** Za 18:17; 1Tim 6:6; Mit 16:8
[b]**15:17** Mit 17:1; Mhu 4:6
[c]**15:18** Mit 14:17; 26:21; Mwa 13:8; Mit 6:16-19; 14:17; Mwa 13:8
[d]**15:19** Mit 22:5
[e]**15:20** Mit 10:1
[f]**15:21** Mit 2:14; 10:23; Efe 5:15
[g]**15:22** Mit 16:7; 1Fal 1:12; Mit 24:6; 11:14
[h]**15:23** Mit 12:14; 25:11
[i]**15:24** Flp 3:20; 3:20
[j]**15:25** Mit 12:7; Kum 19:14; Za 68:5-6; Kum 19:14; Mit 23:10-11
[k]**15:26** Za 59:7
[l]**15:27** Za 15:5; Isa 1:23; Yos 6:18; Zek 5:3; Za 94:11; Mit 6:16; Za 18:27
[m]**15:28** 1Pet 3:15; Mit 14:8
[n]**15:29** Isa 59:2; Efe 2:12; Yn 9:21; Rum 8:26
[o]**15:30** Mit 25:25
[p]**15:31** Mit 9:7-9; 12:1

32 [a]Yeye anayedharau maonyo
hujidharau mwenyewe,
bali yeyote anayekubali maonyo
hupata ufahamu.

33 [b]Kumcha Bwana humfundisha mtu
hekima,
nao unyenyekevu huja kabla ya
heshima.

16 [c]Mipango ya moyoni ni ya
mwanadamu,
bali jibu la ulimi hutoka kwa
Bwana.

2 [d]Njia zote za mtu huonekana safi
machoni pake mwenyewe,
bali makusudi hupimwa na
Bwana.

3 [e]Mkabidhi Bwana lolote ufanyalo,
nayo mipango yako itafanikiwa.

4 [f]Bwana hufanya kila kitu kwa
kusudi lake mwenyewe;
hata waovu kwa siku ya
maangamizi.

5 [g]Bwana huwachukia sana wote
wenye kiburi cha moyo.
Uwe na hakika kwa hili:
Hawataepuka kuadhibiwa.

6 [h]Kwa upendo na uaminifu uovu
huondolewa;
kwa kumcha Bwana mtu
hujiepusha na ubaya.

7 [i]Njia za mtu zinapompendeza
Bwana,
huwafanya hata adui zake waishi
naye kwa amani.

8 [j]Afadhali kitu kidogo pamoja na haki
kuliko mapato mengi pamoja na
udhalimu.

9 [k]Moyo wa mtu huifikiri njia yake,
bali Bwana huelekeza hatua zake.

10 [l]Midomo ya mfalme huzungumza
kwa hekima ya kiungu,
wala kinywa chake hakipotoshi
haki.

11 [m]Vipimo na mizani za halali hutoka
kwa Bwana;
mawe yote ya kupimia yaliyo
katika mfuko ameyafanya
yeye.

12 [n]Wafalme huchukia sana kutenda
maovu,
kwa maana kiti cha ufalme
hufanywa imara kwa njia ya
haki.

13 [o]Wafalme hufurahia midomo ya
uaminifu;
humthamini mtu asemaye kweli.

14 [p]Ghadhabu ya mfalme ni mjumbe wa
mauti,
bali mtu mwenye hekima
ataituliza.

15 [q][r]Uso wa mfalme ung'aapo,
inamaanisha uhai;
upendeleo wake ni kama wingu la
mvua wakati wa vuli.

16 [s]Ni bora kiasi gani kupata hekima
kuliko dhahabu,
kuchagua ufahamu kuliko fedha!

---

[a]**15:32** Mit 1:7; 12:1; Mhu 7:5
[b]**15:33** Mit 29:23; Isa 66:2
[c]**16:1** Mt 10:19; Mit 19:21
[d]**16:2** 1Sam 16:7; 2Nya 6:30; Lk 16:15; Dan 5:27
[e]**16:3** 2Nya 20:20; Za 20:4
[f]**16:4** Isa 43:7; Kut 9:16; 2Nya 34:24; Rum 9:22
[g]**16:5** Za 40:4; Mit 6:16; 11:20-21
[h]**16:6** Kut 20:20; Mit 14:16; Dan 4:26
[i]**16:7** Kol 1:10; Mwa 39:21; Za 105:15; Yer 39:12; 40:1; 42:12; Dan 1:9
[j]**16:8** Za 37:16; Mit 15:16; 17:1; Mhu 4:6
[k]**16:9** Yer 10:23
[l]**16:10** Mit 17:7
[m]**16:11** Law 19:36; Mit 11:1; Eze 45:10
[n]**16:12** Mit 26:28; 25:5; 29:14; 31:5
[o]**16:13** Mit 22:11
[p]**16:14** Mwa 40:2; Ay 29:24
[q]**16:15** 2Nya 36:16; Mit 29:1; Yer 19:11
[r]**16:15** Mwa 40:2; Ay 29:24; Mit 19:12; 25:2-7
[s]**16:16** Za 49:20; Ay 28:15; Mit 3:13-14

17 [a]Njia kuu ya wanyofu huepuka
ubaya;
yeye aichungaye njia yake,
huchunga maisha yake.

18 [b]Kiburi hutangulia maangamizi,
roho ya majivuno hutangulia
maanguko.

19 Ni afadhali kuwa mnyenyekevu
katika roho
miongoni mwa walioonewa
kuliko kugawana nyara pamoja na
wenye kiburi.

20 [c]Yeyote anayekubali mafundisho
hustawi,
tena amebarikiwa yeye
anayemtumaini BWANA.

21 [d]Wenye hekima moyoni huitwa
wenye ufahamu,
na maneno ya kupendeza
huchochea mafundisho.

22 [e]Ufahamu ni chemchemi ya uzima
kwa wale walio nao,
bali upumbavu huleta adhabu kwa
wapumbavu.

23 [f]Moyo wa mtu mwenye hekima
huongoza kinywa chake,
na midomo yake huchochea
mafundisho.

24 [g]Maneno ya kupendeza ni kama sega
la asali,
ni matamu kwa nafsi na uponyaji
kwenye mifupa.

25 [h]Iko njia ionekanayo kuwa sawa kwa
mtu,
bali mwisho wake huelekeza
mautini.

26 [i]Shauku ya mfanyakazi humhimiza
kufanya kazi;
njaa yake humsukuma aendelee.

27 [j]Mtu mbaya kabisa hupanga mabaya,
maneno yake ni kama moto
uunguzao.

28 [k]Mtu mpotovu huchochea ugomvi,
nayo maongezi ya upuzi
hutenganisha marafiki wa
karibu.

29 Mtu mkali humvuta jirani yake
na kumwongoza katika mapito
yale mabaya.

30 [l]Yeye akonyezaye kwa jicho lake
anapanga upotovu;
naye akazaye midomo yake
amenuia mabaya.

31 [m]Mvi ni taji ya utukufu;
hupatikana kwa maisha ya
uadilifu.

32 [n]Ni afadhali mtu mstahimilivu kuliko
shujaa,
mtu anayeitawala hasira yake
kuliko yule autekaye mji.

33 [o]Kura hupigwa kwa siri,
lakini kila uamuzi wake hutoka
kwa BWANA.

17 [p]Afadhali kula ukoko mkavu
ukiwa na amani na utulivu
kuliko kukaa kwenye nyumba ya
karamu kukiwa na magomvi.

2 [q]Mtumishi mwenye hekima atatawala
juu ya mwana aaibishaye,
naye atashirikiana katika urithi
kama mmoja wa hao ndugu.

---

[a]**16:17** Mit 4:24-27; Isa 35:8; Mdo 24:16
[b]**16:18** Es 5:12; Mit 29:23
[c]**16:20** Isa 30:18; Za 32:10; Yer 17:7
[d]**16:21** Mit 16:23
[e]**16:22** Mit 10:11
[f]**16:23** Ay 15:5; Mit 16:21
[g]**16:24** Mit 24:13-14
[h]**16:25** Mit 12:15; 14:12; Es 3:6
[i]**16:26** Mit 9:12; Mhu 6:7
[j]**16:27** Yak 3:6
[k]**16:28** Mit 14:17; 17:9
[l]**16:30** Mit 6:13
[m]**16:31** Mit 20:29
[n]**16:32** Mit 19:11
[o]**16:33** Yos 7:14; Yn 1:7
[p]**17:1** Mit 15:16, 17; 16:8
[q]**17:2** Mit 10:5; 19:26

3 [a]Kalibu ni kwa ajili ya fedha na
tanuru ni kwa ajili ya
dhahabu,
bali Bwana huujaribu moyo.

4 Mtu mwovu husikiliza midomo
mibaya;
mwongo husikiliza kwa makini
ulimi wa madhara.

5 [b]Yeye anaye mdhihaki maskini
huonyesha dharau kwa
Muumba wake;
yeyote afurahiaye maafa
hataepuka kuadhibiwa.

6 [c]Wana wa wana ni taji la wazee,
nao wazazi ni fahari ya watoto
wao.

7 [d]Midomo yenye uwezo wa ushawishi
haimfai mpumbavu:
je, ni mibaya kiasi gani zaidi
midomo ya uongo kwa
mtawala!

8 [e]Kipawa ni kama kito cha thamani
machoni pake yeye aliye
nacho;
kokote kigeukiapo, hufanikiwa.

9 [f]Yeye anayesamehe kosa hudumisha
upendo,
bali yeyote arudiaye jambo
hutenganisha marafiki wa
karibu.

10 Karipio humwingia sana mtu
mwenye kutambua
kuliko mapigo mia kwa
mpumbavu.

11 Mtu mbaya hupenda kuasi tu;
mjumbe asiye na huruma
atatumwa dhidi yake.

[a]**17:3** Mit 27:21; Yer 17:10; 1Pet 1:7; Za 26:2
[b]**17:5** Mit 14:31; Ay 31:39; Eze 25:3; Oba 1:12
[c]**17:6** Za 125:5; Mit 13:22
[d]**17:7** Mit 16:10
[e]**17:8** Mwa 39:21; Dan 6:3
[f]**17:9** Mit 10:12; 16:28

12 [g]Ni afadhali ukutane na dubu
aliyenyang'anywa watoto
wake,
kuliko mpumbavu katika
upumbavu wake.

13 [h]Ikiwa mtu atalipa baya kwa jema,
kamwe ubaya hautaondoka katika
nyumba yake.

14 [i]Kuanzisha ugomvi ni kama kutoboa
bwawa la maji;
kwa hiyo acha jambo hilo kabla
mabishano hayajaanza.

15 [j]Yeye asemaye kuwa asiye na haki
ana haki,
naye asemaye kuwa mwenye haki
hana haki:
Bwana huwachukia sana wote
wawili.

16 [k]Fedha ina faida gani mikononi mwa
mpumbavu,
wakati yeye hana haja ya kupata
hekima?

17 [l]Rafiki hupenda wakati wote
naye ndugu amezaliwa kwa ajili
ya wakati wa shida.

18 [m]Mtu mjinga hupana mkono ili
kuweka rehani,
naye huweka dhamana kwa jirani
yake.

19 Yeye apendaye ugomvi apenda
dhambi;
naye ainuaye sana lango lake[n]
hutafuta uharibifu.

20 Mtu mwenye moyo mpotovu hawezi
kufanikiwa;
naye ambaye ulimi wake ni

[g]**17:12** 1Sam 25:25
[h]**17:13** Yer 18:20; 1Sam 19:4; Rum 12:17; Za 109:4-5
[i]**17:14** Mit 20:3; Mt 5:25-26; Mdo 6:1
[j]**17:15** Za 94:21; Kut 23:6-7; Mit 18:5; Mao 3:34-36; Isa 5:23
[k]**17:16** Mit 23:23
[l]**17:17** 2Sam 15:21; Mit 27:10
[m]**17:18** Mit 6:1-5; 11:5
[n]19 Kuinua lango maana yake ni kusema kwa majivuno.

mdanganyifu huanguka
kwenye taabu.

21 [a]Kuwa na mwana mpumbavu huleta
huzuni;
hakuna furaha kwa baba wa
mpumbavu.

22 [b]Moyo wenye furaha ni dawa nzuri,
bali roho iliyopondeka hukausha
mifupa.

23 [c]Mtu mwovu hukubali rushwa kwa
siri
ili kupotosha njia ya haki.

24 [d]Mtu wa ufahamu huitazama hekima,
lakini macho ya mpumbavu
huhangaika
hadi kwenye miisho ya dunia.

25 [e]Mwana mpumbavu huleta huzuni
kwa baba yake
na uchungu kwa yeye aliyemzaa.

26 [f]Si vizuri kumwadhibu mtu asiye na
hatia,
au kuwapiga sana maafisa kwa
ajili ya uadilifu wao.

27 [g]Mtu mwenye maarifa hutumia
maneno kwa kujizuia,
naye mtu mwenye ufahamu ana
moyo wa utulivu.

28 [h]Hata mtu mpumbavu hudhaniwa
kuwa na hekima kama
akinyamaza,
na mwenye ufahamu kama
akiuzuia ulimi wake.

18 Mtu ajitengaye na wengine
hufuata matakwa yake
mwenyewe;
hupiga vita kila shauri jema.

2 [i]Mpumbavu hafurahii ufahamu,
bali hufurahia kutangaza
maoni yake mwenyewe.

3 Wakati uovu unapokuja, dharau huja
pia,
pamoja na aibu huja lawama.

4 [j]Maneno ya kinywa cha mwanadamu
ni kina cha maji,
bali chemchemi ya hekima ni
kijito kinachobubujika.

5 [k]Sio vizuri kumpendelea mtu mwovu,
au kumnyima haki asiye na hatia.

6 [l]Midomo ya mpumbavu humletea
ugomvi
na kinywa chake hualika kipigo.

7 [m]Kinywa cha mpumbavu ni uharibifu
wake
na midomo yake ni mtego kwa
nafsi yake.

8 [n]Maneno ya mchongezi ni kama
chakula kitamu;
huingia sehemu za ndani sana za
mtu.

9 [o]Mtu aliye mlegevu katika kazi yake
ni ndugu na yule anayeharibu.

10 [p]Jina la BWANA ni ngome imara,
wenye haki huikimbilia na kuwa
salama.

11 [q]Mali ya tajiri ni mji wake wenye
ngome,
wanaudhania kuwa ukuta
usioweza kurukwa.

---

[a]**17:21** Mit 10:1
[b]**17:22** Kut 12:46; Za 22:15
[c]**17:23** Kut 18:21; 1Sam 8:3
[d]**17:24** Ay 31:1; Mhu 2:14
[e]**17:25** Mit 10:1
[f]**17:26** Za 94:21; Mit 18:5
[g]**17:27** Ay 6:24; Mit 14:29
[h]**17:28** Ay 2:13; Mit 10:19
[i]**18:2** Mit 12:23
[j]**18:4** Za 18:16
[k]**18:5** Law 19:15; Mit 28:21; Za 82:2; Ay 13:7-8
[l]**18:6** Mit 10:14
[m]**18:7** Za 140:9; 64:8; Mhu 10:12
[n]**18:8** Mit 26:22
[o]**18:9** Mit 28:24
[p]**18:10** 2Sam 22:3; Za 61:3; 18:2
[q]**18:11** Mit 10:15

12 [a]Kabla ya anguko moyo wa mtu
hujaa kiburi,
bali unyenyekevu hutangulia
heshima.

13 [b]Yeye ajibuye kabla ya kusikiliza,
huo ni upumbavu wake na aibu
yake.

14 [c]Roho ya mtu itastahimili katika
ugonjwa
bali roho iliyovunjika ni nani
awezaye kuistahimili?

15 [d]Moyo wa mwenye ufahamu
hujipatia maarifa,
masikio ya mwenye hekima
huyatafuta maarifa.

16 [e]Zawadi humfungulia njia mtoaji,
nayo humleta mbele ya wakuu.

17 Yeye aliye wa kwanza kuleta
mashtaka huonekana sahihi,
hadi mwingine ajitokezapo na
kumuuliza maswali.

18 Kupiga kura hukomesha mashindano
na kutenganisha wapinzani wakuu
wanaopingana.

19 [f]Ndugu aliyechukizwa ni mgumu
kuridhika
kuliko mji uliozungushiwa ngome,
nayo mabishano ni kama malango
ya ngome yenye makomeo.

20 [g]Tumbo la mtu litajaa kutokana na
tunda la kinywa chake,
atashibishwa mavuno
yanayotokana na midomo
yake.

21 [h]Mauti na uzima viko katika uwezo
wa ulimi,
nao waupendao watakula matunda
yake.

22 [i]Apataye mke apata kitu chema
naye ajipatia kibali kwa BWANA.

23 [j]Mtu maskini huomba kuhurumiwa
bali tajiri hujibu kwa ukali.

24 [k]Mtu mwenye marafiki wengi
wanaweza kumharibu,
bali yuko rafiki aambatanaye na
mtu kwa karibu kuliko ndugu.

19 [l]Afadhali mtu maskini ambaye
mwenendo wake hauna
lawama,
kuliko mpumbavu ambaye
midomo yake imepotoka.

2 [m]Sio vizuri kuwa na juhudi bila
maarifa,
wala kufanya haraka na kuikosa
njia.

3 [n]Upumbavu wa mtu mwenyewe
huharibu maisha yake
hata hivyo moyo wake
humkasirikia BWANA.

4 [o]Mali huleta marafiki wengi,
bali rafiki wa mtu maskini
humwacha.

5 [p]Shahidi wa uongo hataacha
kuadhibiwa,
naye amwagaye uongo hataachwa
huru.

6 [q]Wengi hujipendekeza kwa mtawala
na kila mmoja ni rafiki wa mtu
atoaye zawadi.

---

[a]**18:12** Mit 11:2; 15:33
[b]**18:13** Mit 20:25; Yn 7:51
[c]**18:14** Mit 15:13; 17:22
[d]**18:15** Mit 15:14; Efe 1:17
[e]**18:16** Mwa 32:20; 39:2-6; 41:38-44; 1Sam 10:4
[f]**18:19** 1Sam 17:28
[g]**18:20** Mit 12:14
[h]**18:21** Mit 13:2-3; Mt 12:37
[i]**18:22** Mit 12:4; 31:10; Ay 33:26
[j]**18:23** Mwa 42:13-16; Yak 2:3
[k]**18:24** 1Sam 20:42; Yn 15:13-15
[l]**19:1** Mit 28:6
[m]**19:2** Hos 4:6; Yn 16:3; Rum 10:2
[n]**19:3** Mit 14:1; 9:13; 24:9; Isa 32:6; Yak 1:13-15
[o]**19:4** Mit 19:7; 14:20
[p]**19:5** Kut 23:1; Kum 19:19; Mit 1:28
[q]**19:6** Mit 29:26; 17:8; 18:16

7 [a]Mtu maskini huepukwa na ndugu
zake wote:
Je, marafiki zake watamkwepa
kiasi gani!
Ingawa huwafuata kwa kuwasihi,
hawapatikani popote.

8 [b]Yeye apataye hekima huipenda nafsi
yake mwenyewe,
yeye ahifadhiye ufahamu hustawi.

9 [c]Shahidi wa uongo hataacha
kuadhibiwa,
naye amwagaye uongo
ataangamia.

10 [d]Haistahili mpumbavu kuishi katika
anasa,
itakuwa vibaya kiasi gani
kwa mtumwa kuwatawala wakuu.

11 [e]Hekima ya mtu humpa uvumilivu,
ni kwa utukufu wake kusamehe
makosa.

12 [f]Ghadhabu ya mfalme ni kama
mngurumo wa simba,
bali wema wake ni kama umande
juu ya nyasi.

13 [g]Mwana mpumbavu ni maangamizi
ya babaye,
naye mke mgomvi ni kama
kutonatona kusikoisha.

14 [h]Nyumba na mali hurithiwa kutoka
kwa wazazi,
bali mke mwenye busara hutoka
kwa BWANA.

15 [i]Uvivu huleta usingizi mzito,
naye mtu mzembe huona njaa.

16 [j]Yeye ambaye hutii mafundisho
huulinda uhai wake,
bali yeye anayezidharau njia zake
atakufa.

17 [k]Yeye amhurumiaye maskini
humkopesha BWANA,
naye atamtuza kwa aliyotenda.

18 [l]Mrudi mwanao, kwa maana katika
hiyo kuna tumaini,
usiwe mshirika katika mauti yake.

19 Mtu mwenye kukasirika haraka ni
lazima atapata adhabu yake,
kama utamwokoa, itakubidi
kufanya hivyo tena.

20 [m]Sikiliza mashauri na ukubali
mafundisho,
nawe mwishoni utakuwa na
hekima.

21 [n]Kuna mipango mingi ndani ya moyo
wa mtu,
lakini kusudi la BWANA ndilo
litakalosimama.

22 Lile mtu alionealo shauku ni upendo
usio na mwisho,
afadhali kuwa maskini kuliko
kuwa mwongo.

23 [o]Kumcha BWANA huongoza kwenye
uzima,
kisha mtu hupumzika akiwa
ameridhika,
bila kuguswa na shida.

24 [p]Mtu mvivu hutumbukiza mkono
wake kwenye sahani,
lakini hawezi hata kuupeleka
kwenye kinywa chake!

[a]**19:7** Mit 10:15
[b]**19:8** Mit 16:20
[c]**19:9** Kum 19:19
[d]**19:10** Mit 26:1; 30:21-23; Mhu 10:5-7
[e]**19:11** 2Fal 5:12; Mit 16:32; Mt 25:21; Efe 4:32
[f]**19:12** Za 33:3; 72:5-6; Es 1:12
[g]**19:13** Mit 10:1; Es 1:18; Mit 21:9
[h]**19:14** 2Kor 12:14; Mit 18:22
[i]**19:15** Mit 10:4; 20:13
[j]**19:16** Mit 16:17; Lk 10:28; Rum 2:7
[k]**19:17** Kum 24:19; Mt 10:42; 2Kor 9:6
[l]**19:18** Mit 13:24; 23:13-14
[m]**19:20** Mit 4:1; 12:15
[n]**19:21** Es 9:25; Mhu 7:29; Yer 4:29; Mao 3:37; Ebr 6:17
[o]**19:23** Za 25:13; 1Tim 4:8; Ay 4:7; Mit 10:27
[p]**19:24** Mit 26:15

25 [a]Mpige mwenye mzaha, naye mjinga
atajifunza busara,
mkemee mwenye ufahamu naye
atapata maarifa.

26 [b]Yeye amwibiaye baba yake na
kumfukuza mama yake
ni mwana aletaye aibu na fedheha.

27 [c]Mwanangu, ukiacha kusikiliza
mafundisho,
utatangatanga mbali na maneno
ya maarifa.

28 [d]Shahidi mla rushwa hudhihaki
hukumu
na kinywa cha mtu mwovu
humeza ubaya kwa upesi.

29 [e]Adhabu zimeandaliwa kwa ajili ya
wenye dhihaka
na mapigo kwa ajili ya migongo
ya wapumbavu.

20 [f]Mvinyo ni mdhihaki na kileo ni
mgomvi;
yeyote apotoshwaye navyo hana
hekima.

2 [g]Ghadhabu ya mfalme ni kama
ngurumo ya simba;
yeye amkasirishaye hupoteza uhai
wake.

3 [h]Ni kwa heshima ya mtu kujitenga
ugomvi,
bali kila mpumbavu ni mwepesi
kugombana.

4 [i]Mvivu halimi kwa majira;
kwa hiyo wakati wa mavuno
hutazama
lakini hapati chochote.

5 [j]Makusudi ya moyo wa mwanadamu
ni maji yenye kina,
lakini mtu mwenye ufahamu
huyachota.

6 [k]Watu wengi hujidai kuwa na
upendo usiokoma,
bali mtu mwaminifu ni nani
awezaye kumpata?

7 [l]Mtu mwenye haki huishi maisha
yasiyo na lawama,
wamebarikiwa watoto wake baada
yake.

8 [m]Wakati mfalme aketipo katika kiti
chake cha enzi kuhukumu,
hupepeta ubaya wote kwa macho
yake.

9 [n]Ni nani awezaye kusema,
"Nimeuweka moyo wangu
safi;
mimi ni safi na sina dhambi?"

10 [o]Mawe ya kupimia yaliyo tofauti na
vipimo tofauti,
Bwana huchukia vyote viwili.

11 [p]Hata mtoto hujulikana kwa matendo
yake,
kama tabia yake ni safi na adili.

12 [q]Masikio yasikiayo na macho
yaonayo,
Bwana ndiye alivifanya vyote
viwili.

13 [r]Usiupende usingizi la sivyo utakuwa
maskini,
uwe macho nawe utakuwa na
chakula cha akiba.

14 "Haifai, haifai!" asema mnunuzi,
kisha huondoka akijisifia ununuzi
wake.

---

[a] **19:25** Za 141:5; Mit 9:9; 21:11
[b] **19:26** Mit 28:24
[c] **19:27** Mt 7:15; Mk 4:24; Efe 4:14
[d] **19:28** Ay 15:16
[e] **19:29** Kum 25:2; Mit 26:3
[f] **20:1** Law 10:9; Hab 2:5; 1Sam 25:36; 1Fal 20:16; Mit 31:4
[g] **20:2** Mit 8:36; 19:12; Es 7:7
[h] **20:3** Mwa 13:8; Mit 17:14
[i] **20:4** Mit 6:6; Mhu 10:18
[j] **20:5** Za 18:16
[k] **20:6** Za 12:1; Mt 6:2; Mhu 7:28; Lk 18:8
[l] **20:7** Za 26:1; 37:25-26; 112:2
[m] **20:8** 1Fal 7:7; Mit 25:4-5
[n] **20:9** Mhu 7:20; 1Fal 8:46; 1Yn 1:8
[o] **20:10** Mit 20:23; 11:1
[p] **20:11** Za 39:1; Mt 7:16
[q] **20:12** Kut 4:11; Rum 11:26; Za 94:9
[r] **20:13** Mit 6:11; 19:15; Rum 12:11

15 [a]Dhahabu kunayo, na marijani kwa wingi,
lakini midomo inenayo maarifa
ni kito cha thamani kilicho adimu.

16 [b]Chukua vazi la yule awekaye dhamana
kwa ajili ya mgeni;
lishikilie iwe dhamana kama anafanya hivyo
kwa ajili ya mwanamke mpotovu.

17 Chakula kilichopatikana kwa hila ni kitamu kwa mwanadamu,
bali huishia na kinywa kilichojaa changarawe.

18 [c]Fanya mipango kwa kutafuta mashauri,
ukipigana vita, tafuta maelekezo.

19 [d]Maneno ya kusengenya husababisha kutokuaminika,
kwa hiyo mwepuke mtu anayezungumza kupita kiasi.

20 [e]Ikiwa mtu atamlaani baba yake au mama yake,
taa yake itazimwa katika giza nene.

21 [f]Urithi upatikanao haraka mwanzoni,
hautabarikiwa mwishoni.

22 [g]Usiseme, "Nitakulipiza kwa ajili ya kosa hili!"
Mngojee BWANA, naye atakuokoa.

23 [h]BWANA anachukia sana mawe ya kupimia ya udanganyifu,
nazo mizani zisizo halali hazimpendezi.

24 [i]Hatua za mtu huongozwa na BWANA.
Anawezaje basi mtu yeyote kuelewa njia yake mwenyewe?

25 [j]Ni mtego kwa mtu kuweka wakfu kitu kwa haraka
na baada ya kitambo kidogo kufikiria tena nadhiri zake.

26 [k]Mfalme mwenye hekima hupepeta waovu,
hulipitisha gurudumu la kupuria juu yao.

27 [l]Taa ya BWANA huchunguza roho ya mwanadamu,
huchunguza utu wake wa ndani.

28 [m]Upendo na uaminifu humweka mfalme salama,
kwa njia ya upendo, kiti chake cha enzi huwa salama.

29 [n]Utukufu wa vijana ni nguvu zao,
mvi ni fahari ya uzee.

30 [o]Mapigo na majeraha huusafisha ubaya,
nayo michapo hutakasa utu wa ndani.

21 [p]Moyo wa mfalme uko katika mkono wa BWANA;
huuongoza kama mkondo wa maji, popote apendapo.

2 [q]Njia zote za mwanadamu huonekana sawa kwake,
bali BWANA huupima moyo.

3 [r]Kufanya yaliyo sawa na haki inakubalika
zaidi kwa BWANA kuliko dhabihu.

[a]**20:15** Ay 28:12, 16, 17, 18, 19
[b]**20:16** Kut 22:26; Mit 27:13
[c]**20:18** Mit 11:14; 24:6
[d]**20:19** Mit 11:13
[e]**20:20** Kut 21:17; Mit 30:11; Ay 18:5; Law 20:9
[f]**20:21** Mit 28:8; Hab 2:6
[g]**20:22** Mit 24:29; Yer 42:11; Kum 32:35; Rum 12:17-19
[h]**20:23** Kum 25:13
[i]**20:24** Mit 19:21; Yer 10:23; Rum 8:26
[j]**20:25** Mhu 5:2-5; Yer 44:25
[k]**20:26** Mit 20:8
[l]**20:27** Za 119:105; Mit 16:2
[m]**20:28** Mit 29:14; Isa 16:5
[n]**20:29** Mit 16:31
[o]**20:30** Za 51:2; Mit 22:15
[p]**21:1** Es 5:1; Yer 39:11-12
[q]**21:2** Mit 24:12; Lk 16:15; Yer 17:10; 1Sam 16:7
[r]**21:3** Hos 6:6; Mik 6:6-8

4 [a]Macho ya kudharau na moyo wa kiburi,
ambavyo ni taa ya waovu, vyote ni dhambi!

5 [b]Mipango ya mwenye bidii huelekeza kwenye faida,
kama vile kwa hakika pupa huelekeza kwenye umaskini.

6 [c]Mali iliyopatikana kwa ulimi wa uongo
ni mvuke upitao upesi na mtego wa kufisha.

7 [d]Jeuri ya waovu itawaburuta mbali,
kwa kuwa wanakataa kufanya yaliyo sawa.

8 [e]Njia ya mwenye hatia ni ya upotovu,
bali tabia ya mtu asiye na hatia ni nyofu.

9 [f]Ni afadhali kuishi pembeni mwa paa la nyumba,
kuliko kuishi nyumba moja na mke mgomvi.

10 [g]Mtu mwovu hutamani sana ubaya,
jirani yake hapati huruma kutoka kwake.

11 [h]Wakati mwenye mzaha ameadhibiwa,
mjinga hupata hekima;
wakati mtu mwenye hekima afundishwapo,
hupata maarifa.

12 [i]Mwenye Haki huyajua yanayotendeka katika nyumba za waovu,
naye atawaangamiza waovu.

13 [j]Mtu akiziba masikio asisikie kilio cha maskini,
yeye pia atalia, wala hatajibiwa.

14 [k]Zawadi itolewayo kwa siri hutuliza hasira
na rushwa iliyofichwa kwenye nguo hutuliza ghadhabu kali.

15 [l]Wakati haki imetendeka, huleta furaha kwa wenye haki,
bali kitisho kwa watenda mabaya.

16 [m]Mtu anayepotea kutoka mapito ya ufahamu,
hupumzika katika kundi la waliokufa.

17 [n]Mtu apendaye anasa atakuwa maskini,
yeyote apendaye mvinyo na mafuta kamwe hatakuwa tajiri.

18 [o]Waovu huwa fidia kwa ajili ya wenye haki,
nao wasio waaminifu kwa ajili ya wanyofu.

19 [p]Ni afadhali kuishi jangwani
kuliko kuishi na mke mgomvi na mkorofi.

20 [q]Katika nyumba ya mwenye hekima
kuna akiba ya vyakula vizuri na mafuta,
lakini mtu mpumbavu
hutafuna vyote alivyo navyo.

21 [r]Yeye afuatiaye haki na upendo
hupata uzima, mafanikio na heshima.

---

[a]**21:4** Ay 41:34; Mit 6:17
[b]**21:5** Mit 10:4
[c]**21:6** Mit 10:2; 2Pet 2:3
[d]**21:7** Mit 11:5
[e]**21:8** Mit 2:15
[f]**21:9** Mit 21:19; 19:13; 25:24
[g]**21:10** Yak 4:5
[h]**21:11** Mit 19:25
[i]**21:12** 1Kor 10:10; Rum 2:8; Mit 14:11
[j]**21:13** Ay 29:12; Zek 7:11; Mdo 7:57; Yak 2:13
[k]**21:14** Mwa 32:20; Mit 18:16
[l]**21:15** Mit 21:9
[m]**21:16** Za 49:14; Eze 18:24
[n]**21:17** Mit 23:20-21, 29-35
[o]**21:18** Isa 43:3-4; Mit 11:8
[p]**21:19** Mit 21:9
[q]**21:20** Za 112:3; Mit 10:22; Mt 25:3
[r]**21:21** 1Kor 15:58; Za 25:13; Mt 5:6

[22] [a]Mtu mwenye hekima huushambulia
mji wa wenye nguvu,
na kuangusha ngome
wanazozitegemea.

[23] [b]Yeye alindaye kinywa chake na
ulimi wake
hujilinda na maafa.

[24] [c]Mtu mwenye kiburi na majivuno,
"Mdhihaki" ndilo jina lake;
hutenda mambo kwa kiburi
kilichozidi.

[25] [d]Kutamani sana kwa mvivu
kutakuwa kifo chake,
kwa sababu mikono yake haitaki
kufanya kazi.

[26] [e]Mchana kutwa hutamani zaidi,
lakini mnyofu hutoa pasipo
kuzuia.

[27] [f]Dhabihu ya mtu mwovu ni chukizo,
si zaidi sana itolewapo kwa nia
mbaya!

[28] [g]Shahidi wa uongo ataangamia,
bali maneno ya mwenye kusikia
yatadumu.

[29] [h]Mtu mwovu ana uso wa ushupavu,
bali mtu mnyofu huzifikiria njia
zake.

[30] [i]Hakuna hekima, wala akili, wala
mpango
unaoweza kufaulu dhidi ya
BWANA.

[31] [j]Farasi huandaliwa kwa ajili ya siku
ya vita,
bali ushindi huwa kwa BWANA.

# 22

[1] [k]Heri kuchagua jina jema kuliko
utajiri mwingi,
kuheshimiwa ni bora kuliko fedha
au dhahabu.

[2] [l]Tajiri na maskini wanafanana kwa
hili:
BWANA ni Muumba wao wote.

[3] [m]Mtu mwenye busara huona hatari
na kujificha,
bali mjinga huendelea mbele kama
kipofu nayo ikamtesa.

[4] [n]Unyenyekevu na kumcha BWANA
huleta utajiri, heshima na uzima.

[5] [o]Katika mapito ya waovu kuna miiba
na mitego,
bali yeye ailindaye nafsi yake
hukaa mbali nayo.

[6] [p]Mfundishe mtoto njia impasayo
kuiendea,
naye hataiacha hata akiwa mzee.

[7] [q]Matajiri huwatawala maskini
naye akopaye ni mtumwa wa
akopeshaye.

[8] [r]Yeye aupandaye uovu huvuna
taabu,
nayo fimbo ya ghadhabu yake
itaangamizwa.

[9] [s]Mtu mkarimu yeye mwenyewe
atabarikiwa
kwa kuwa hushiriki chakula chake
na maskini.

[10] [t]Mfukuze mwenye dhihaka,
na mvutano utatoweka;
ugomvi na matukano vitakoma.

---

[a]**21:22** Mit 8:14; Mhu 9:15-16
[b]**21:23** Za 34:13; Yak 3:2; Mit 12:13
[c]**21:24** Yer 43:2
[d]**21:25** Mit 13:4
[e]**21:26** Law 25:35; Mt 5:42
[f]**21:27** 1Fal 14:24; Amo 5:22; Mit 15:8
[g]**21:28** Isa 29:21; Mit 19:5
[h]**21:29** Mit 14:8
[i]**21:30** Ay 12:13; Yer 9:23; 2Nya 13:12; Mdo 5:39
[j]**21:31** Isa 31:1; Za 3:8
[k]**22:1** Mhu 7:1
[l]**22:2** Ay 31:15; Mt 5:45; Za 49:1-2
[m]**22:3** Mit 14:16; 27:12; Isa 26:20
[n]**22:4** Mit 15:33; 10:27; Dan 4:36
[o]**22:5** Mit 15:19; 1Yn 5:18
[p]**22:6** Efe 6:4
[q]**22:7** Yak 2:6
[r]**22:8** Hos 10:13; 8:7; Kut 1:20; Gal 6:7-8; Za 125:3
[s]**22:9** Kum 14:29; 2Kor 9:6; Mit 11:25; 28:27
[t]**22:10** Mit 26:20; Mwa 21:9, 10; Za 101:5

11 [a]Yeye apendaye moyo safi na yeye
ambaye maneno yake ni ya
neema,
mfalme atakuwa rafiki yake.

12 Macho ya BWANA hulinda maarifa,
bali huyapinga maneno ya asiye
mwaminifu.

13 [b]Mvivu husema, "Yuko simba nje!"
au, "Nitauawa katika mitaa!"

14 [c]Kinywa cha mwanamke kahaba ni
shimo refu;
yeye aliye chini ya ghadhabu ya
BWANA
atatumbukia ndani yake.

15 [d]Upumbavu umefungwa ndani ya
moyo wa mtoto,
bali fimbo ya adhabu itaufukuzia
mbali naye.

16 [e]Yeye amwoneaye maskini ili
kujiongezea mali,
naye ampaye tajiri zawadi, wote
huwa maskini.

*Misemo Ya Wenye Hekima*

17 [f]Tega sikio na usikie misemo ya
wenye hekima,
elekeza moyo wako kwenye yale
nifundishayo,
18 kwa maana inapendeza
unapoyahifadhi moyoni
mwako
na kuwa nayo yote tayari
midomoni mwako.
19 Ili tumaini lako liwe katika BWANA,
hata wewe, ninakufundisha leo.
20 [g]Je, sijakuandikia misemo thelathini,
misemo ya mashauri na maarifa,
21 [h]kukufundisha maneno ya kweli na
ya kuaminika,
ili uweze kutoa majibu sahihi
kwake yeye aliyekutuma?

22 [i]Usiwadhulumu maskini kwa sababu
ni maskini,
wala kumdhulumu mhitaji
mahakamani,
23 [j]kwa sababu BWANA atalichukua
shauri lao
naye atawateka wao waliowateka.

24 Usifanye urafiki na mtu mwenye
hasira ya haraka,
usishirikiane na yule aliye
mwepesi kukasirika,
25 [k]la sivyo utajifunza njia zake
na kujiingiza mwenyewe kwenye
mtego.

26 [l]Usiwe mwenye kupana mikono
katika rehani,
au kuweka dhamana kwa ajili ya
madeni.
27 [m]Kama ukikosa njia ya kulipa,
kitanda chako
kitachukuliwa ukiwa umekilalia.

28 [n]Usisogeze jiwe la mpaka wa zamani
lililowekwa na baba zako.

29 [o]Je, unamwona mtu stadi katika kazi
yake?
Atahudumu mbele ya wafalme;
hatahudumu mbele ya watu duni.

23 Uketipo kula chakula na mtawala,
angalia vyema kile
kilicho mbele yako,
2 na utie kisu kooni mwako
kama ukiwa mlafi.
3 [p]Usitamani vyakula vyake vitamu
kwa kuwa chakula hicho ni cha
hila.

---

[a]**22:11** Mit 16:13; Mt 5:8
[b]**22:13** Mit 26:13
[c]**22:14** Mit 6:12; Mhu 7:26
[d]**22:15** Mit 13:24; 20:30
[e]**22:16** Ay 20:19-23; Amo 2:6-8; Isa 3:14-15; Yak 2:13
[f]**22:17** Mit 1:8; 1:6; 30:1; 31:1; 2:2
[g]**22:20** Mit 8:6
[h]**22:21** 1Pet 3:15; Mhu 12:10
[i]**22:22** Law 25:17; Zek 7:10; Kut 23:6; Mal 3:5
[j]**22:23** Ay 29:16; Za 12:5; 1Sam 25:39
[k]**22:25** 1Kor 15:33
[l]**22:26** Kum 19:14; Mit 23:10
[m]**22:27** Mit 11:15; 17:18
[n]**22:28** Kum 19:14
[o]**22:29** 1Fal 11:28; Mwa 41:46; Mhu 9:10
[p]**23:3** Za 141:4

4 [a]Usijitaabishe ili kuupata utajiri,
uwe na hekima kuonyesha kujizuia.
5 [b]Kufumba na kufumbua utajiri hutoweka,
huwa kama umepata mabawa ghafula,
ukaruka na kutoweka angani kama tai.

6 [c]Usile chakula cha mtu mchoyo,
usitamani vyakula vyake vitamu,
7 [d]kwa maana yeye ni aina ya mtu
ambaye kila mara anafikiri juu ya gharama.
Anakuambia, "Kula na kunywa,"
lakini moyo wake hauko pamoja nawe.
8 Utatapika kile kidogo ulichokula,
nawe utakuwa umepoteza bure
maneno yako ya kumsifu.

9 [e]Usizungumze na mpumbavu,
kwa maana atadhihaki hekima ya maneno yako.

10 [f]Usisogeze jiwe la mpaka wa zamani
wala kunyemelea kwenye mashamba ya yatima,
11 [g]kwa kuwa Mtetezi wao ni mwenye nguvu,
atalichukua shauri lao dhidi yako.

12 [h]Elekeza moyo wako kwenye mafundisho
na masikio yako kwenye maneno ya maarifa.

13 [i]Usimnyime mtoto adhabu,
ukimwadhibu kwa fimbo, hatakufa.
14 [j]Mwadhibu kwa fimbo
na kuiokoa nafsi yake kutoka mautini.[k]

15 [l]Mwanangu, kama moyo wako una hekima,
basi moyo wangu utafurahi,
16 [m]utu wangu wa ndani utafurahi,
wakati midomo yako
itakapozungumza lililo sawa.

17 [n]Usiuruhusu moyo wako kuwaonea wivu wenye dhambi,
bali kila mara uwe na bidii katika kumcha BWANA.
18 [o]Hakika kuna tumaini la baadaye kwa ajili yako,
nalo tarajio lako halitakatiliwa mbali.

19 [p]Sikiliza, mwanangu na uwe na hekima,
weka moyo wako kwenye njia iliyo sawa.
20 [q]Usiwe miongoni mwa wanywao mvinyo,
au wale walao nyama kwa pupa,
21 [r]kwa maana walevi na walafi huwa maskini,
nako kusinzia huwavika matambara.

22 [s]Msikilize baba yako, aliyekuzaa,
wala usimdharau mama yako atakapokuwa mzee.
23 [t]Nunua kweli wala usiiuze,
pata hekima, adabu na ufahamu.
24 [u]Baba wa mwenye haki ana furaha kubwa,
naye aliye na mwana mwenye hekima humfurahia.

---

[a]**23:4** Yn 6:27; 1Tim 6:9; Rum 12:16
[b]**23:5** Mt 6:19; Mit 27:24
[c]**23:6** Za 141:4; Kum 15:9
[d]**23:7** Za 12:2
[e]**23:9** Mit 9:7
[f]**23:10** Kum 19:14; Mit 22:28
[g]**23:11** Ay 19:25; Kut 22:22-24; Yer 50:34; Mit 15:25
[h]**23:12** Mit 2:2
[i]**23:13** Mit 13:24; 19:18; 22:18; 22:15; 29:15, 16
[j]**23:14** Mit 13:24; 19:18
[k]14 Mautini maana yake ni Kuzimu.
[l]**23:15** Mit 23:24, 25; 29:3
[m]**23:16** Mit 23:24
[n]**23:17** Za 73:3; Mit 28:14
[o]**23:18** Za 37:1-4; Mit 24:14-20
[p]**23:19** Kum 4:9; Mit 28:7
[q]**23:20** Hab 2:15; Rum 13:13; Isa 5:22
[r]**23:21** Mit 21:17; 19:23; 19:15
[s]**23:22** Law 19:32; Efe 6:1-2
[t]**23:23** Mit 4:7; 17:16; Mt 13:44
[u]**23:24** Mit 23:15-16; 10:1; 15:20

25 [a]Baba yako na mama yako na
wafurahi,
mama aliyekuzaa na ashangilie!

26 [b]Mwanangu, nipe moyo wako,
macho yako na yafuate njia zangu,
27 [c]kwa maana kahaba ni shimo refu
na mwanamke mpotovu ni kisima
chembamba.
28 [d]Kama mnyang'anyi, hungojea
akivizia,
naye huzidisha wasio waaminifu
miongoni mwa wanaume.

29 [e]Ni nani mwenye ole?
Ni nani mwenye huzuni?
Ni nani mwenye ugomvi?
Ni nani mwenye malalamiko?
Ni nani aliye na majeraha yasiyo na
sababu?
Ni nani mwenye macho mekundu?
30 [f]Ni hao wakaao sana kwenye
mvinyo,
hao waendao kuonja mabakuli ya
mvinyo uliochanganywa.
31 Usiukodolee macho mvinyo wakati
ukiwa mwekundu,
wakati unapometameta kwenye
bilauri,
wakati ushukapo taratibu!
32 Mwishowe huuma kama nyoka
na kutia sumu yake kama nyoka
mwenye sumu.
33 Macho yako yataona mambo mageni
na moyo wako kuwazia mambo
yaliyopotoka.
34 Utakuwa kama alalaye katikati ya
bahari,
alalaye juu ya kamba ya merikebu.
35 [g]Utasema, "Wamenipiga lakini
sikuumia!
Wamenichapa, lakini sisikii!
Nitaamka lini
ili nikanywe tena?"

24 [h]Usiwaonee wivu watu waovu,
usitamani ushirika
nao;
2 [i]kwa maana mioyo yao hupanga
mambo ya jeuri,
nayo midomo yao husema juu ya
kuleta madhara.

3 [j]Kwa hekima nyumba hujengwa,
nayo kwa njia ya ufahamu
huimarishwa
4 [k]kwa njia ya maarifa vyumba vyake
hujazwa
vitu vya thamani na vya
kupendeza.

5 [l]Mtu mwenye hekima ana uwezo
mkubwa,
naye mtu mwenye maarifa
huongeza nguvu,
6 [m]kwa kufanya vita unahitaji uongozi
na kwa ushindi washauri wengi.

7 [n]Hekima i juu mno kwa mpumbavu,
katika kusanyiko langoni
hana lolote la kusema.

8 [o]Yeye apangaye mabaya
atajulikana kama mtu wa hila.
9 [pq]Mipango ya upumbavu ni dhambi,
watu huchukizwa na mwenye
dhihaka.

---

[a]**23:25** Mit 10:1
[b]**23:26** Mit 5:1-6; Za 18:21
[c]**23:27** Mit 22:14
[d]**23:28** Mit 7:11-12; Mhu 7:26
[e]**23:29** 1Fal 20:16; Mit 20:1; Isa 5:11; Nah 1:10; Mt 24:49, 50; Efe 5:18
[f]**23:30** Za 75:8; Efe 5:18; Mit 20:1; Efe 5:18; Za 75:8; Mit 9:2
[g]**23:35** Mit 27:22; Yer 5:3; Kum 29:19; Isa 56:12; 2Pet 2:22
[h]**24:1** Mit 3:31-32; 23:17-18
[i]**24:2** Za 2:1; 10:7; Isa 32:6; 55:7-8; 59:7; 65:2; Hos 4:1
[j]**24:3** Mit 14:1
[k]**24:4** Mit 8:21
[l]**24:5** Mit 21:22
[m]**24:6** Mit 11:14; Lk 14:31
[n]**24:7** Za 10:5; Mit 14:6
[o]**24:8** Rum 1:30
[p]**24:9** Mwa 6:5; Za 119:113; Mt 9:4; Mdo 8:22; 2Kor 10:5
[q]**24:9** Mwa 6:5; Mdo 8:22; 2Kor 10:5

10 [a]Ukikata tamaa wakati wa taabu,
jinsi gani nguvu zako ni kidogo!
11 [b]Okoa wale wanaoongozwa kwenye kifo;
wazuie wote wanaojikokota kuelekea machinjoni.
12 [c]Kama mkisema, "Lakini hatukujua lolote kuhusu hili,"
je, yule apimaye mioyo halitambui hili?
Je, yule awalindaye maisha yenu halijui hili?
Je, hatamlipa kila mtu kulingana na aliyotenda?

13 [d]Ule asali mwanangu, kwa kuwa ni nzuri;
asali kutoka kwenye sega ni tamu kwa kuonja.
14 [e]Ujue pia kwamba hekima ni tamu kwa nafsi yako,
kama ukiipata, kuna matumaini kwako ya siku zijazo,
nalo tumaini lako halitakatiliwa mbali.

15 [f]Usivizie kama haramia afanyavyo ili kuyashambulia
makao ya mwenye haki,
wala usiyavamie makazi yake,
16 [g]Kwa maana ingawa mtu mwenye haki huanguka mara saba, huinuka tena,
lakini waovu huangushwa chini na maafa.

17 [h]Usitazame kwa kufurahia adui yako aangukapo;
wakati ajikwaapo,
usiruhusu moyo wako ushangilie.
18 [i]BWANA asije akaona na kuchukia
akaiondoa ghadhabu yake mbali naye.

19 [j]Usikasirike kwa sababu ya watu wabaya
wala usiwaonee wivu waovu,
20 [k]kwa maana mtu mbaya hana tumaini la siku zijazo,
nayo taa ya waovu itazimwa.

21 [l]Mwanangu, mche BWANA na mfalme,
wala usijiunge na waasi,
22 [m]kwa maana hao wawili watatuma maangamizi ya ghafula juu yao,
naye ni nani ajuaye maafa wawezayo kuleta?

*Misemo Zaidi Ya Wenye Hekima*

23 [n]Hii pia ni misemo ya wenye hekima:

Kuonyesha upendeleo katika hukumu si vyema:
24 [o]Yeyote amwambiaye mwenye hatia, "Wewe huna hatia,"
Kabila zitamlaani
na mataifa yatamkana.
25 Bali itakuwa vyema kwa wale watakaowatia hatiani wenye hatia,
nazo baraka tele zitawajilia juu yao.

26 Jawabu la uaminifu
ni kama busu la midomoni.

27 [p]Maliza kazi zako za nje,
nawe uweke mashamba yako tayari,
baada ya hayo, jenga nyumba yako.

---

[a]**24:10** Yer 51:46; Ebr 12:3
[b]**24:11** Isa 58:6-7; 1Yn 3:16; Za 82:4
[c]**24:12** Za 139:2; Mit 16:24; 21:2; Yer 32:19; Mt 16:24
[d]**24:13** Wim 5:1
[e]**24:14** Za 119:103; Mit 16:24; 23:18
[f]**24:15** Za 10:9, 10
[g]**24:16** Ay 5:19; Mik 7:8; Za 34:19
[h]**24:17** Oba 1:12; Ay 31:29
[i]**24:18** Ay 31:29
[j]**24:19** Za 37:1
[k]**24:20** Ay 18:5; Mit 13:9; Isa 3:11
[l]**24:21** Rum 13:1-7; 1Pet 2:17
[m]**24:22** Za 73:19
[n]**24:23** Kut 18:16; Law 19:15; 2Nya 19:7; Za 72:2; Yer 22:16; Yn 7:24
[o]**24:24** Isa 5:23; Mit 17:15
[p]**24:27** 1Fal 5:17, 18; Lk 14:28

28 [a]Usishuhudie dhidi ya jirani yako
bila sababu,
au kutumia midomo yako
kudanganya.
29 [b]Usiseme, "Nitamtenda kama
alivyonitenda mimi;
nitamlipiza mtu yule kwa kile
alichonitendea."

30 [c]Nilipita karibu na shamba la mvivu,
karibu na shamba la mizabibu la
mtu asiye na akili,
31 [d]miiba ilikuwa imeota kila mahali,
ardhi ilikuwa imefunikwa na
magugu, na
ukuta wa mawe ulikuwa
umebomoka.
32 Nikatafakari moyoni mwangu lile
nililoliona,
nami nikajifunza somo kutokana
na niliyoyaona:
33 [e]Bado kulala kidogo, kusinzia
kidogo,
bado kukunja mikono kidogo
upate kupumzika:
34 [f]hivyo umaskini utakuja juu yako
kama mnyang'anyi,
na kupungukiwa kutakujia kama
mtu mwenye silaha.

### *Mithali Zaidi Za Solomoni*

25 [g]Hizi ni mithali zaidi za Solomoni, zilizonakiliwa na watu wa Hezekia mfalme wa Yuda:

2 [h]Ni Utukufu wa Mungu kuficha
jambo,
bali ni utukufu wa wafalme
kuchunguza jambo.

3 Kama mbingu zilivyo juu na nchi
ilivyo chini,
ndivyo ambavyo mioyo ya
wafalme haichunguziki.

4 [i]Ondoa takataka kwenye madini ya
fedha,
nako ndani yake kutatokea
chombo
cha mfua fedha.
5 [j]Ondoa waovu mbele ya mfalme,
nacho kiti chake cha enzi
kitaimarishwa kwa njia ya haki.

6 Usijikweze mwenyewe mbele ya
mfalme,
wala usidai nafasi miongoni mwa
watu wakuu;
7 [k]ni afadhali yeye akuambie, "Njoo
huku juu,"
kuliko yeye kukuaibisha mbele ya
mkuu.

Kile ulichokiona kwa macho yako
8 [l]usiharakishe kukipeleka
mahakamani,
maana utafanya nini mwishoni
kama jirani yako atakuaibisha?

9 [m]Kama ukifanya shauri na jirani
yako,
usisaliti siri ya mtu mwingine,
10 ama yeye aisikiaye aweza
kukuaibisha
na kamwe sifa yako mbaya
haitaondoka.

11 [n]Neno lisemwalo kwa wakati ufaao
ni kama matunda ya mtofaa ya
dhahabu
yaliyowekwa kwenye vijalizo vya
fedha.

12 [o]Kama vile kipuli cha dhahabu
au pambo la dhahabu safi,
ndivyo lilivyo karipio la mtu
mwenye hekima
kwa sikio lisikilizalo.

[a]**24:28** Za 7:4; Efe 4:25
[b]**24:29** Mit 20:22; Rum 12:17; Mt 5:39
[c]**24:30** Mit 6:6-11; 26:13-16
[d]**24:31** Yer 4:3; Ebr 6:8
[e]**24:33** Mit 6:10
[f]**24:34** Mit 10:4; Mhu 10:18
[g]**25:1** 1Fal 4:32
[h]**25:2** Kum 29:29; Rum 11:33; Mit 10:10-15
[i]**25:4** 2Tim 2:21
[j]**25:5** 2Sam 7:13; Mit 20:8; 29:14
[k]**25:7** Lk 14:7-10
[l]**25:8** Mit 17:14; Mt 5:25-26
[m]**25:9** Mt 5:25; 18:15
[n]**25:11** Mit 15:23; Isa 50:4
[o]**25:12** Za 141:5; Mit 15:31

13 [a]Kama vile ubaridi wa theluji wakati wa mavuno
ndivyo alivyo mjumbe mwaminifu kwa wale wamtumao,
huburudisha roho za bwana zake.

14 [b]Kama vile mawingu na upepo pasipo mvua
ndivyo alivyo mtu ajisifuye kwa zawadi ambazo hatoi.

15 [c]Kwa njia ya uvumilivu mtawala aweza kushawishiwa,
nao ulimi laini waweza kuvunja mfupa.

16 [d]Ukipata asali, kula kiasi tu cha kukutosha,
ukila zaidi, utatapika.
17 Ingiza mguu wako nyumbani kwa jirani yako mara chache,
ukizidisha, atakukinai na atakuchukia.

18 [e]Kama vile rungu au upanga au mshale mkali
ndivyo alivyo mtu atoaye ushuhuda wa uongo dhidi ya jirani yake.

19 [f]Kama vile jino bovu au mguu uliolemaa,
ndivyo ilivyo kumtegemea mtu asiye mwaminifu wakati wa shida.

20 [g]Kama vile avuaye mavazi siku ya baridi,
au kama siki iliyomwagwa juu ya magadi,
ndivyo alivyo yeye amuimbiaye nyimbo mtu mwenye moyo mzito.

21 [h]Kama adui yako ana njaa, mpe chakula ale;
kama ana kiu, mpe maji anywe.
22 [i]Kwa kufanya hivyo, unaweka makaa ya moto yanayowaka kichwani pake,
naye BWANA atakupa thawabu.

23 [j]Kama vile upepo wa kaskazini uletavyo mvua,
ndivyo ulimi usingiziao uletavyo uso wa hasira.

24 [k]Ni afadhali kuishi pembeni mwa paa la nyumba,
kuliko kuishi nyumba moja na mke mgomvi.

25 Kama vile maji baridi kwa nafsi iliyochoka
ndivyo zilivyo habari njema kutoka nchi ya mbali.

26 [l]Kama vile chemchemi iliyotibuliwa matope au
kisima kilichotiwa taka
ndivyo alivyo mtu mwenye haki
akishiriki na waovu.

27 [m]Si vyema kula asali nyingi sana,
wala si heshima
kujitafutia heshima yako mwenyewe.

28 [n]Kama vile mji ambao kuta zake zimebomoka
ndivyo alivyo mtu
ambaye hawezi kujitawala mwenyewe.

26 1 [o]Kama theluji wakati wa kiangazi au mvua wakati wa mavuno,
ndivyo asivyostahili heshima mpumbavu.

[a]**25:13** Mit 13:17; 10:26
[b]**25:14** Mit 20:6; Yud 12
[c]**25:15** Mhu 10:4; Mit 15:1; Mwa 32:4; 1Sam 25:24
[d]**25:16** Mit 25:27
[e]**25:18** Za 57:4; Mit 12:18
[f]**25:19** Ay 6:14-20; 2Tim 4:16
[g]**25:20** Dan 6:18; Rum 12:15
[h]**25:21** Kut 23:4; Mt 5:44; Rum 12:20
[i]**25:22** 2Sam 16:22; Mt 5:44; Za 18:8
[j]**25:23** Ay 37:22; Za 105:5
[k]**25:24** Mit 19:13; 21:9, 19
[l]**25:26** Mik 7:8
[m]**25:27** Mit 27:2; Mt 23:12; Lk 14:11
[n]**25:28** Mit 16:32
[o]**26:1** Isa 32:6; 1Sam 12:17; Mit 19:10

2 [a]Kama shomoro apigapigavyo
mabawa yake
au mbayuwayu katika kuruka
kwake kasi,
ndivyo ilivyo laana isiyo na
sababu haimpati mtu.

3 [b]Mjeledi kwa farasi, lijamu kwa
punda,
nayo fimbo kwa migongo ya
wapumbavu!

4 [c]Usimjibu mpumbavu sawasawa na
upumbavu wake,
ama wewe mwenyewe utakuwa
kama yeye.

5 [d]Mjibu mpumbavu sawasawa na
upumbavu wake,
ama atakuwa mwenye hekima
machoni pake mwenyewe.

6 [e]Kama vile ilivyo kujikata miguu au
kunywa hasara,
ndivyo ilivyo kutuma ujumbe kwa
mkono wa mpumbavu.

7 [f]Kama miguu ya kiwete
inavyoning'inia
ndivyo ilivyo mithali katika
kinywa cha mpumbavu.

8 [g]Kama kufunga jiwe kwenye
kombeo,
ndivyo ilivyo kumpa mpumbavu
heshima.

9 [h]Kama mwiba kwenye mkono wa
mlevi
ndivyo ilivyo mithali kinywani
mwa mpumbavu.

10 Kama mpiga upinde ambaye
hujeruhi ovyo,
ndivyo alivyo yeye aajiriye
mpumbavu au yeyote apitaye
njiani.

11 [i]Kama mbwa ayarudiavyo matapiko
yake,
ndivyo mpumbavu arudiavyo
upumbavu wake.

12 [j]Je, unamwona mtu ajionaye
mwenye hekima
machoni pake mwenyewe?
Liko tumaini zaidi kwa mpumbavu
kuliko kwake.

13 [k]Mvivu husema, "Yuko simba
barabarani,
simba mkali anazunguka mitaa!"

14 [l]Kama vile mlango ugeukavyo
kwenye bawaba zake,
ndivyo mvivu ajigeuzavyo
kitandani mwake.

15 [m]Mtu mvivu hutumbukiza mkono
wake kwenye sahani,
naye huchoka kuupeleka kwenye
kinywa chake.

16 Mtu mvivu ni mwenye hekima
machoni pake mwenyewe,
kuliko watu saba wawezao kujibu
kwa busara.

17 Kama yeye amkamataye mbwa kwa
masikio,
ndivyo alivyo mtu apitaye njiani
na kujiingiza kwenye ugomvi
usiomhusu.

18 Kama mtu mwendawazimu
atupaye vijinga vya moto au
mishale ya kufisha,
19 [n]ndivyo alivyo mtu amdanganyaye
jirani yake na kusema,
"Nilikuwa nikifanya mzaha tu!"

20 [o]Bila kuni moto huzimika;
pasipo uchongezi ugomvi
humalizika.

[a]**26:2** Hes 23:8; Kum 23:5
[b]**26:3** Za 32:9; Mit 10:13
[c]**26:4** Isa 36:21
[d]**26:5** Mt 16:14; 21:24-27; Mit 3:7
[e]**26:6** Mit 10:26
[f]**26:7** Mit 26:9
[g]**26:8** Mit 26:1
[h]**26:9** Mit 26:7
[i]**26:11** Kut 8:15; Za 85:8; 2Pet 2:22
[j]**26:12** Ufu 3:17; Mit 29:20
[k]**26:13** Mit 6:6-11; 24:30-34; 22:13
[l]**26:14** Mit 6:9
[m]**26:15** Mit 19:24
[n]**26:19** Efe 5:4
[o]**26:20** Mit 22:10

21 [a]Kama makaa juu ya makaa
yanayowaka, na kama kuni
kwenye moto,
ndivyo alivyo mtu mgomvi kwa
kuchochea ugomvi.

22 [b]Maneno ya mchongezi ni kama
chakula kitamu;
huingia sehemu za ndani sana za
mtu.

23 [c]Kama rangi ing'aayo iliyopakwa
kwenye vyombo vya udongo
ndivyo ilivyo midomo laini
pamoja na moyo mbaya.

24 [d]Mtu mwenye nia ya kudhuru
wengine hujificha kwa
maneno ya midomo yake,
lakini moyoni mwake huficha
udanganyifu.
25 [e]Ingawa maneno yake huvutia,
usimwamini,
kwa maana machukizo saba
hujaza moyo wake.
26 Nia yake ya kudhuru wengine
inaweza kufichwa na
udanganyifu,
lakini uovu wake utafichuliwa
kwenye kusanyiko.

27 [f]Kama mtu akichimba shimo,
atatumbukia ndani yake,
kama mtu akivingirisha jiwe,
litamrudia.

28 [g]Ulimi wa uongo, huwachukia wale
unaowaumiza,
nacho kinywa cha kujipendekeza
hutenda uharibifu.

27 1 [h]Usijisifu kwa ajili ya kesho,
kwa kuwa hujui ni
nini kitakachozaliwa kwa siku
moja.

2 [i]Mwache mwingine akusifu,
wala si kinywa chako mwenyewe;
mtu mwingine afanye hivyo
na si midomo yako mwenyewe.

3 [j]Jiwe ni zito na mchanga ni mzigo,
lakini kukasirishwa na mpumbavu
ni kuzito kuliko vyote viwili.

4 [k]Hasira ni ukatili na ghadhabu kali ni
gharika,
lakini ni nani awezaye kusimama
mbele ya wivu?

5 [l]Afadhali karipio la wazi
kuliko upendo uliofichika.

6 [m]Majeraha kutoka kwa rafiki
yaonyesha uaminifu,
bali kubusu kwa adui ni kwingi
sana.

7 [n]Yeye aliyeshiba huchukia kabisa
asali,
bali kwa mwenye njaa
hata kile kilicho kichungu
kwake ni kitamu.

8 [o]Kama ndege atangatangavyo mbali
na kiota chake,
ndivyo alivyo mtu atangatangaye
mbali na nyumbani mwake.

9 [p]Manukato na uvumba huleta furaha
moyoni,
nao uzuri wa rafiki huchipuka
kutoka kwenye ushauri wake wa
uaminifu.

---

[a]**26:21** Mit 14:17
[b]**26:22** Mit 18:8; Eze 22:9
[c]**26:23** Lk 22:48
[d]**26:24** Za 31:18; 41:6; Mit 10:18; Za 31:18; 41:6
[e]**26:25** Za 28:3; Yer 9:4-8
[f]**26:27** Za 7:15-16; 35:8; Mhu 10:8; Mit 28:10; Es 6:13; 7:9
[g]**26:28** Mit 13:6; 29:5; Za 12:3
[h]**27:1** Lk 12:19-20; Yak 4:13; Mt 6:34; 1Fal 20:11
[i]**27:2** Mit 25:27
[j]**27:3** Ay 6:3; Es 1:12
[k]**27:4** 1Yn 3:12
[l]**27:5** Gal 2:14
[m]**27:6** Za 141:5; Mit 28:23
[n]**27:7** Ay 6:7
[o]**27:8** Isa 16:2; Ay 39:14
[p]**27:9** Es 2:12; Za 45:8

10 [a]Usimwache rafiki yako wala rafiki
wa baba yako,
tena usiende nyumbani mwa
ndugu yako
wakati umepatwa na maafa.
Bora jirani wa karibu
kuliko ndugu aliye mbali.

11 [b]Mwanangu, uwe na hekima,
nawe ulete furaha moyoni
mwangu,
ndipo nitakapoweza kumjibu yeyote
anitendaye kwa dharau.

12 [c]Mtu mwenye busara huona hatari
na kujificha,
bali mjinga huendelea mbele nayo
ikamtesa.

13 [d]Chukua vazi la yule awekaye
dhamana
kwa ajili ya mgeni;
lishikilie iwe dhamana kama
anafanya hivyo
kwa ajili ya mwanamke mpotovu.

14 [e]Kama mtu akimbariki jirani yake
kwa sauti kuu
asubuhi na mapema,
itahesabiwa kama ni laana.

15 [f]Mke mgomvi ni kama
matone yasiyokoma ya siku ya
mvua.
16 Kumzuia yeye ni kama kuuzuia
upepo
au kukamata mafuta kwa kiganja
cha mkono.

17 Kama vile chuma kinoavyo chuma,
ndivyo mtu amnoavyo mwenzake.

18 [g]Yeye autunzaye mtini atakula tunda
lake,
naye amtunzaye bwana wake
ataheshimiwa.

19 Kama uso uonekanavyo kwenye
maji,
ndivyo hivyo moyo wa mtu
humwonyesha alivyo.

20 [h]Kuzimu na Uharibifu havishibi
kadhalika macho ya mwanadamu.

21 [i]Kalibu ni kwa ajili ya fedha
na tanuru kwa ajili ya dhahabu,
bali mtu hupimwa kwa sifa
azipokeazo.

22 [j]Hata ukimtwanga mpumbavu
kwenye kinu,
ukimtwanga kama nafaka kwa
mchi,
hutauondoa upumbavu wake.

23 [k]Hakikisha kuwa unajua hali ya
makundi yako
ya kondoo na mbuzi,
angalia kwa bidii ng'ombe zako.
24 [l]Kwa kuwa utajiri haudumu milele,
nayo taji haidumu vizazi vyote.
25 [m]Wakati majani makavu
yameondolewa
na mapya yamechipua,
nayo majani toka milimani
yamekusanywa,
26 wana-kondoo watakupatia mavazi
na mbuzi thamani ya shamba.
27 Utakuwa na maziwa mengi ya mbuzi
kukulisha wewe na jamaa yako,
na kuwalisha watumishi wako wa
kike.

28

1 [n]Mtu mwovu hukimbia ingawa
hakuna yeyote anayemfukuza,
bali wenye haki ni wajasiri kama
simba.

2 Wakati nchi inapokuwa na uasi,
inakuwa na viongozi wengi,
bali mwenye ufahamu na maarifa
hudumisha utaratibu.

---

[a]**27:10** Mit 17:17
[b]**27:11** Mit 10:1; 23:15-16; Mwa 24:60
[c]**27:12** Mit 22:3
[d]**27:13** Mit 20:16
[e]**27:14** Za 12:2
[f]**27:15** Es 1:18; Mit 19:13
[g]**27:18** 1Kor 9:7; Lk 19:12-27; Kum 20:6
[h]**27:20** Mit 30:15-16; Hab 2:5; Mhu 6:7
[i]**27:21** Mit 17:3
[j]**27:22** Isa 1:5; Yer 5:3; Mit 23:35
[k]**27:23** Mit 12:10; Yer 5:3
[l]**27:24** Mit 23:5
[m]**27:25** Za 104:14
[n]**28:1** 2Fal 7:7; Law 26:17; Za 53:5

3 [a]Mtu maskini amwoneaye yeye aliye
maskini zaidi
ni kama mvua ya dhoruba
isiyosaza mazao.

4 [b]Wale waiachao sheria huwasifu
waovu,
bali wale waishikao sheria
huwapinga.

5 [c]Watu wabaya hawaelewi haki,
bali wale wamtafutao BWANA
wanaielewa kikamilifu.

6 [d]Afadhali maskini ambaye
mwenendo wake hauna
lawama
kuliko tajiri ambaye njia zake ni
potovu.

7 [e]Yeye ashikaye sheria ni mwana
mwenye ufahamu,
bali rafiki wa walafi humwaibisha
baba yake.

8 [f]Yeye aongezaye utajiri wake kwa
riba kubwa mno
hukusanya kwa ajili ya mwingine,
ambaye atawahurumia maskini.

9 [g]Kama mtu yeyote akikataa kusikia
sheria,
hata maombi yake ni chukizo.

10 [h]Yeye ambaye humwongoza mwenye
haki kwenye mapito mabaya,
ataanguka kwenye mtego wake
mwenyewe,
bali wasio na lawama watapokea
urithi mwema.

11 Mtu tajiri anaweza kuwa na hekima
machoni pake mwenyewe,
bali mtu maskini mwenye
ufahamu atamfichua.

12 [i]Mwenye haki ashindapo, kuna
furaha kubwa,
bali waovu watawalapo, watu
hujificha.

13 [j]Yeye afichaye dhambi zake
hatafanikiwa,
bali yeyote aziungamaye na
kuziacha hupata rehema.

14 [k]Amebarikiwa mtu ambaye siku zote
humcha BWANA,
bali yeye afanyaye moyo wake
kuwa mgumu
huangukia kwenye taabu.

15 Kama simba angurumaye au dubu
ashambuliaye,
ndivyo alivyo mtu mwovu
atawalaye wanyonge.

16 Mtawala dhalimu hana akili,
bali yeye achukiaye mapato ya
udhalimu
atafurahia maisha marefu.

17 [l]Mtu mwenye kusumbuliwa na hatia
ya kuua
atakuwa mtoro mpaka kufa;
mtu yeyote na asimsaidie.

18 [m]Yeye ambaye mwenendo wake
hauna lawama
hulindwa salama,
bali yeye ambaye njia zake ni potovu
ataanguka ghafula.

19 [n]Yeye alimaye shamba lake atakuwa
na chakula tele,
bali yule afuataye mambo ya
upuzi atakuwa na umaskini
wa kumtosha.

20 [o]Mtu mwaminifu atabarikiwa sana,
bali yeye atamaniye kupata utajiri
kwa haraka
hataacha kuadhibiwa.

[a]**28:3** Mt 18:28
[b]**28:4** 1Fal 18:18; Mt 3:7; Efe 5:11; 1Tim 5:20
[c]**28:5** Yn 7:17; 1Kor 2:15
[d]**28:6** Mit 19:1
[e]**28:7** Mit 23:19-21
[f]**28:8** Ay 27:16-17; Eze 18:8; Kut 18:21; Mit 13:22; Lk 14:12-14
[g]**28:9** Za 66:18; Zek 7:11; Isa 1:13; 2Tim 4:3
[h]**28:10** Za 34:9; 57:6; Mk 10:30; Mit 26:27; Rum 8:32
[i]**28:12** 2Fal 11:20; Ay 24:4; Mit 11:10
[j]**28:13** 1Yn 1:8-10; 2Sam 12:13; Ay 31:33; Dan 4:27
[k]**28:14** Za 16:8; Mit 23:17; Rum 2:5; 11:20
[l]**28:17** Mwa 9:6; 1Sam 30:17
[m]**28:18** Es 6:13; Mit 10:9
[n]**28:19** Mit 12:11
[o]**28:20** Mit 13:11; 20:21; 23:4, 22; 1Tim 6:9

21 [a]Kuonyesha upendeleo si vizuri,
hata hivyo mtu atafanya kosa kwa kipande cha mkate.

22 [b]Mtu mchoyo ana tamaa ya kupata utajiri,
naye hana habari kuwa umaskini unamngojea.

23 [c]Yeye amkemeaye mtu mwishoni hupata kibali zaidi,
kuliko mwenye maneno ya kusifu isivyostahili.

24 [d]Yeye amwibiaye babaye au mamaye
na kusema, "Si kosa,"
yeye ni mwenzi wa yule aharibuye.

25 [e]Mtu mwenye tamaa huchochea fitina,
bali yule amtegemeaye Bwana atafanikiwa.

26 [f]Yeye ajitumainiaye mwenyewe ni mpumbavu,
bali yeye atembeaye katika hekima hulindwa salama.

27 [g]Yeye ampaye maskini
hatapungukiwa na kitu chochote,
bali yeye awafumbiaye maskini macho
hupata laana nyingi.

28 [h]Wakati waovu watawalapo,
watu huenda mafichoni,
bali waovu wanapoangamia,
wenye haki hufanikiwa.

## 29

1 [i]Mtu anayeendelea kuwa na shingo ngumu baada ya maonyo mengi,
ataangamia ghafula, wala hapati dawa.

2 [j]Wenye haki wanapostawi, watu hufurahi;
waovu watawalapo, watu hulia kwa huzuni.

3 [k]Mtu apendaye hekima huleta furaha kwa baba yake,
bali aambatanaye na makahaba hutapanya mali yake.

4 [l]Kwa haki mfalme huipa nchi uthabiti,
bali mfalme aliye na tamaa ya rushwa huiangamiza.

5 [m]Yeyote amsifuye jirani yake isivyostahili,
anautandaza wavu kuitega miguu yake.

6 [n]Mtu mbaya hutegwa na dhambi yake mwenyewe
bali mwenye haki huweza kuimba na kufurahi.

7 [o]Mwenye haki hujali haki kwa ajili ya maskini,
bali mwovu hajishughulishi na hilo.

8 [p]Wenye mzaha huuchochea mji,
bali watu wenye hekima hugeuzia mbali hasira.

9 [q]Kama mwenye hekima akienda mahakamani na mpumbavu,
mpumbavu hukasirika na kudhihaki, wala hakuna amani.

10 [r]Watu wamwagao damu humchukia mtu mwadilifu
na hutafuta kumuua mtu mnyofu.

---

[a]**28:21** Eze 13:19; Za 94:21; Mit 18:5
[b]**28:22** Mit 28:20
[c]**28:23** Mit 27:5, 6
[d]**28:24** Mit 18:9; 19:26
[e]**28:25** 1Tim 6:6; Mit 29:25
[f]**28:26** Za 4:5; Mit 3:5
[g]**28:27** Kum 15:7; Mit 19:17; 22:9
[h]**28:28** Mit 28:12; Ay 20:19
[i]**29:1** 2Nya 36:16; Mit 6:15
[j]**29:2** 2Fal 11:20; Es 8:15; Mit 28:12
[k]**29:3** 1Fal 1:48; Mit 10:1; 23:15-16; 5:8-10; Lk 15:11-32
[l]**29:4** Mit 8:15-16
[m]**29:5** Ay 32:21; Mit 26:28
[n]**29:6** Ay 5:13; Mhu 9:12
[o]**29:7** Ay 29:16; Za 41:1; Isa 35:3-4
[p]**29:8** Mit 11:11; 16:14
[q]**29:9** Mt 11:17
[r]**29:10** Mwa 4:5-8; 1Yn 3:12

11 [a]Mpumbavu huonyesha hasira yake
yote,
bali mwenye hekima hujizuia.

12 [b]Kama mtawala akisikiliza uongo,
maafisa wake wote huwa waovu.

13 [c]Mtu maskini na mtu anayeonea
wanafanana kwa jambo hili:
BWANA hutia nuru macho yao
wote wawili.

14 [d]Kama mfalme akiwaamua maskini
kwa haki,
kiti chake cha enzi kitakuwa
thabiti siku zote.

15 [e]Fimbo ya maonyo hutia hekima,
bali mtoto aliyeachiwa bila
maonyo
humwaibisha mama yake.

16 [f]Wakati waovu wanapostawi,
pia dhambi vivyo hivyo,
lakini wenye haki wataliona
anguko lao.

17 [g]Mrudi mwanao, naye atakupa
amani,
atakufurahisha nafsi yako.

18 [h]Mahali pasipo na ufunuo, watu
kujizuia,
bali ana heri mtu yule aishikaye
sheria.

19 Mtumishi hawezi kuonywa kwa
maneno matupu,
ajapoelewa, hataitikia.

20 [i]Je, unamwona mtu azungumzaye
kwa haraka?
Kuna matumaini zaidi kwa
mpumbavu kuliko yeye.

21 Kama mtu akimdekeza mtumishi
wake tangu ujanani,
atamletea sikitiko mwishoni.

22 [j]Mtu mwenye hasira huchochea
ugomvi,
naye mtu mwenye hasira ya
haraka
hutenda dhambi nyingi.

23 [k]Kiburi cha mtu humshusha,
bali mtu mwenye roho ya
unyenyekevu
hupata heshima.

24 [l]Anayekubaliana na mwizi ni adui
wa nafsi yake mwenyewe;
huapishwa lakini hathubutu
kushuhudia.

25 [m]Kuwaogopa watu huwa ni mtego,
bali yeyote amtumainiaye BWANA
atakuwa salama.

26 [n]Wengi hutafuta kusikilizwa na
mtawala,
bali mtu hupata haki kutoka kwa
BWANA.

27 [o]Mwenye haki huwachukia sana
wasio waaminifu;
waovu huwachukia sana wenye
haki.

*Misemo Ya Aguri*

30 [p]Misemo ya Aguri mwana wa Yake,
usia:

Huyu mtu alimwambia Ithieli,
naam, kwa Ithieli na kwa Ukali:

2 [q]"Mimi ni mjinga kuliko wanadamu
wote;
sina ufahamu wa kibinadamu.

---

[a]**29:11** Ay 15:13; Mit 12:16
[b]**29:12** 2Fal 21:9; Ay 34:30
[c]**29:13** Mit 22:2; Mt 5:45
[d]**29:14** Mit 29:4; Za 72:1-5; Mit 16:12
[e]**29:15** Mit 29:17; 13:24
[f]**29:16** Za 37:36; 58:10; 91:8
[g]**29:17** Mit 13:24; 29:15
[h]**29:18** Za 19:11; Yn 13:17; Amo 8:11-12; 1Sam 3:1
[i]**29:20** Mit 14:17
[j]**29:22** Mit 14:17
[k]**29:23** Isa 66:2; Mt 23:12; Yak 4:6
[l]**29:24** Law 5:1
[m]**29:25** 1Sam 15:24; Mit 28:25; 16:20
[n]**29:26** Mit 19:6; 16:33
[o]**29:27** Mit 29:10
[p]**30:1** Mit 22:17
[q]**30:2** Za 73:22

3 [a]Sijajifunza hekima,
wala sina maarifa ya kumjua yeye Aliye Mtakatifu.
4 [b]Ni nani ameshapanda mbinguni na kushuka?
Ni nani ameshakusanya upepo kwenye vitanga vya mikono yake?
Ni nani ameshafungia maji kwenye nguo yake?
Ni nani ameimarisha miisho yote ya dunia?
Jina lake ni nani, na mwanawe anaitwa nani?
Niambie kama unajua!

5 [c]"Kila neno la Mungu ni kamilifu;
yeye ni ngao kwa wale wanaomkimbilia.
6 [d]Usiongeze kwenye maneno yake,
ama atakukemea na kukuthibitisha kuwa mwongo.

7 "Ninakuomba vitu viwili, Ee BWANA;
usininyime kabla sijafa:
8 [e]Uutenge mbali nami udanganyifu na uongo;
usinipe umaskini wala utajiri,
bali unipe chakula cha kunitosha kila siku.
9 [f]Nisije nikawa na vingi vya kuzidi nikakukana
na kusema, 'BWANA ni nani?'
Au nisije nikawa maskini nikaiba,
nami nikaliaibisha jina la Mungu wangu.

10 "Usimchongee mtumishi kwa bwana wake,
asije akakulaani, ukapatilizwa kwalo.

11 [g]"Wako watu wale ambao huwalaani baba zao
na wala hawawabariki mama zao;
12 [h]wale ambao ni safi machoni pao wenyewe
kumbe hawakuoshwa uchafu wao;
13 [i]wale ambao daima macho yao ni ya kiburi,
ambao kutazama kwao ni kwa dharau;
14 [j]wale ambao meno yao ni panga
na ambao mataya yao yamewekwa visu
kuwaangamiza maskini katika nchi,
na wahitaji kutoka miongoni mwa wanadamu.

15 [k]"Mruba anao binti wawili waliao,
'Nipe! Nipe!'

"Kuna vitu vitatu visivyotosheka kamwe,
naam, viko vinne visivyosema, 'Yatosha!':
16 [l]Ni kaburi, tumbo lisilozaa,
nchi isiyoshiba maji kamwe,
na moto, usiosema kamwe, 'Yatosha!'

17 [m]"Jicho lile limdhihakilo baba,
lile linalodharau kumtii mama,
litang'olewa na kunguru wa bondeni,
litaliwa na tai.

18 "Kuna vitu vitatu vinavyonishangaza sana,
naam, vinne nisivyovielewa:
19 Ni mwendo wa tai katika anga,
mwendo wa nyoka juu ya mwamba,
mwendo wa meli katika maji makuu ya bahari,
nao mwendo wa mtu pamoja na msichana.

---

[a]**30:3** Mit 9:10
[b]**30:4** Kum 30:12; Ufu 19:12; Yn 3:13; Ay 26:8; Efe 4:7-10
[c]**30:5** Za 18:30; 12:6; 84:11
[d]**30:6** Kum 12:32; Ufu 22:18
[e]**30:8** Mt 6:18
[f]**30:9** Neh 9:25; Kum 6:12; 8:12; Yos 24:27; Hos 13:6
[g]**30:11** Mit 20:20
[h]**30:12** Lk 18:11; Mit 16:2; Yer 2:23-35
[i]**30:13** Ay 41:34
[j]**30:14** Ay 24:9; 29:17; Za 14:4; 57:4; Amo 8:4; Mik 2:2
[k]**30:15** Mit 27:20
[l]**30:16** Isa 5:14; Hab 2:5
[m]**30:17** Kum 21:18-21; Mit 20:20; Law 20:9; Ay 15:23

20 [a]"Huu ndio mwendo wa mwanamke mzinzi,
hula akapangusa kinywa chake na kusema,
'Sikufanya chochote kibaya.'

21 "Kwa mambo matatu nchi hutetemeka,
naam, kwa mambo manne haiwezi kuvumilia:
22 [b]Mtumwa awapo mfalme,
mpumbavu ashibapo chakula,
23 mwanamke asiyependwa aolewapo,
naye mtumishi wa kike achukuapo nafasi ya bibi yake.

24 "Vitu vinne duniani vilivyo vidogo,
lakini vina akili nyingi sana:
25 [c]Mchwa ni viumbe wenye nguvu ndogo,
hata hivyo hujiwekea akiba ya chakula chao wakati wa kiangazi.
26 [d]Pelele ni viumbe vyenye uwezo mdogo
hata hivyo hujitengenezea nyumba zao kwenye miamba.
27 [e]Nzige hawana mfalme,
hata hivyo huenda pamoja vikosi vikosi.
28 Mjusi anaweza kushikwa kwa mkono,
hata hivyo huonekana katika majumba ya kifalme.

29 "Viko vitu vitatu ambavyo vinapendeza katika mwendo wao,
naam, vinne ambavyo hutembea kwa mwendo wa madaha:
30 simba, mwenye nguvu miongoni mwa wanyama,
asiyerudi nyuma kwa chochote;
31 jogoo atembeaye kwa maringo, pia beberu,
naye mfalme pamoja na jeshi lake lililomzunguka.

32 [f]"Ikiwa umefanya upumbavu na ukajitukuza mwenyewe,
au kama umepanga mabaya,
basi funika mdomo wako na mkono wako.
33 Kwa maana kama vile kusukasuka maziwa hutoa siagi,
na pia kule kufinya pua hutoa damu,
kadhalika kuchochea hasira hutokeza ugomvi."

*Misemo Ya Mfalme Lemueli*

31 [g]Misemo ya Mfalme Lemueli, usia wa mama yake aliyomfundisha:

2 [h]"Ee mwanangu, ee mwana wa tumbo langu,
ee mwana wa nadhiri zangu,[i]
3 [j]Usitumie nguvu zako kwa wanawake,
uhodari wako kwa wale wanaowaharibu wafalme.

4 [k]"Ee Lemueli, haifai wafalme,
haifai wafalme kunywa mvinyo,
haifai watawala kutamani sana kileo,
5 [l]wasije wakanywa na kusahau vile sheria inavyoamuru
na kuwanyima haki zao wote walioonewa.
6 [m]Wape kileo wale wanaoangamia,
mvinyo wale walio na uchungu,
7 [n]Wanywe na kusahau umaskini wao
na wasikumbuke taabu yao tena.

8 [o]"Sema kwa ajili ya wale wasioweza kujisemea,
kwa ajili ya haki za wote walioachwa ukiwa.

[a]**30:20** Mit 5:6
[b]**30:22** Mit 19:10; 29:2; Mhu 10:7
[c]**30:25** Mit 6:6-8
[d]**30:26** Za 104:18
[e]**30:27** Kut 10:4
[f]**30:32** Ay 21:5; 29:9; Mhu 8:3; Mik 7:16
[g]**31:1** Mit 22:17
[h]**31:2** Amu 11:30; Isa 49:15
[i]2 Au: Ewe uliye jibu la maombi yangu.
[j]**31:3** Neh 13:26; Kum 17:17; Hos 4:11; 1Fal 11:3
[k]**31:4** Mhu 10:17; Isa 5:22
[l]**31:5** 1Fal 16:9; Mit 16:12; Hos 4:11
[m]**31:6** Mwa 14:18
[n]**31:7** Es 1:10
[o]**31:8** 1Sam 19:4; Es 4:16; Ay 29:12-17

9 [a]Sema na uamue kwa haki,
tetea haki za maskini na wahitaji.”

*Maneno Ya Mwisho: Mke Mwenye Sifa Nzuri*

10 [b]Mke mwenye sifa nzuri, ni nani
awezaye kumpata?
Yeye ni wa thamani sana kuliko
marijani.[c]
11 [d]Mume wake anamwamini kikamilifu
wala hakosi kitu chochote cha
thamani.
12 Humtendea mumewe mema, wala si
mabaya,
siku zote za maisha yake.
13 [e]Huchagua sufu na kitani
naye hufanya kazi kwa mikono
yenye bidii.
14 Yeye ni kama meli za biashara
akileta chakula chake kutoka
mbali.
15 [f]Yeye huamka kungali bado giza
huwapa jamaa yake chakula
na mafungu kwa watumishi wake
wa kike.
16 Huangalia shamba na kulinunua,
kutokana na mapato yake hupanda
shamba la mizabibu.
17 Hufanya kazi zake kwa nguvu,
mikono yake ina nguvu kwa ajili
ya kazi zake.
18 Huona kwamba biashara yake ina
faida,
wala taa yake haizimiki usiku.
19 Huweka mikono yake kwenye pia,
navyo vidole vyake hushikilia
kijiti chenye uzi.
20 [g]Huwanyooshea maskini mikono
yake
na kuwakunjulia wahitaji vitanga
vyake.
21 [h]Theluji ishukapo, hana hofu kwa
ajili ya watu wa nyumbani
mwake,
kwa maana wote wamevikwa
nguo za kutia joto.
22 Hutengeneza mazulia ya urembo ya
kufunika kitanda chake,
yeye huvaa kitani safi na urujuani.
23 [i]Mume wake anaheshimiwa kwenye
lango la mji,
aketipo miongoni mwa wazee wa
nchi.
24 Hutengeneza mavazi ya kitani na
kuyauza,
naye huwauzia wafanyabiashara
mishipi.
25 [j]Amevikwa nguvu na heshima,
anaweza kucheka bila kuwa na
hofu kwa siku zijazo.
26 Huzungumza kwa hekima
na mafundisho ya kuaminika yapo
ulimini mwake.
27 [k]Huangalia mambo ya nyumbani
mwake
wala hali chakula cha uvivu.
28 [l]Watoto wake huamka na kumwita
aliyebarikiwa,
mumewe pia humsifu, akisema:
29 “Wanawake wengi hufanya vitu
vyenye sifa nzuri,
lakini wewe umewapita wote.”
30 [m]Kujipamba ili kuvutia ni
udanganyifu na uzuri unapita
upesi,
bali mwanamke anayemcha
BWANA atasifiwa.

---

[a]**31:9** Law 19:15; Yer 22:16; Kum 1:16; Isa 1:17
[b]**31:10** Rut 3:11; Mit 19:14
[c]10 Mithali 31:10-31 imetungwa kila mstari ukianzia na herufi ya alfabeti ya Kiebrania zikifuatana tangu Aleph (A) hadi Taw (T); zote ni 22.
[d]**31:11** Mwa 2:18; Mit 12:4
[e]**31:13** 1Tim 2:9-10
[f]**31:15** Mt 24:45; Rum 12:11; Ay 23:12
[g]**31:20** Kum 15:11; Ebr 13:16; Efe 4:26-28
[h]**31:21** Yos 2:18-19; Ebr 9:19-22
[i]**31:23** Kut 3:16; Kum 16:18; Rut 4:1, 11; Mit 12:4
[j]**31:25** 1Tim 2:9, 10
[k]**31:27** Mit 14:1; 1Tim 5:14; 2Tim 3:15; Tit 2:4-5
[l]**31:28** 1Fal 2:19
[m]**31:30** Za 112:1

31 Mpe thawabu anayostahili,
nazo kazi zake na zimletee sifa
kwenye lango la mji.

# MHUBIRI

*Kila Kitu Ni Ubatili Mtupu*

1 [a]Maneno ya Mhubiri, mwana wa Daudi,
mfalme huko Yerusalemu:

2 [b]"Ubatili mtupu! Ubatili mtupu!"
Mhubiri anasema.
"Ubatili mtupu!
Kila kitu ni ubatili."

3 [c]Mwanadamu anafaidi nini kutokana
na kazi yake yote
anayotaabikia chini ya jua?
4 [d]Vizazi huja na vizazi hupita,
lakini dunia inadumu milele.
5 [e]Jua huchomoza na jua huzama,
nalo huharakisha kurudi mawioni.
6 Upepo huvuma kuelekea kusini
na kugeukia kaskazini,
hurudia mzunguko huo huo,
daima ukirudia njia yake.
7 [f]Mito yote hutiririka baharini,
hata hivyo bahari kamwe haijai.
Mahali mito inapotoka,
huko hurudi tena.
8 [g]Vitu vyote vinachosha,
zaidi kuliko mtu anavyoweza
kusema.
Jicho kamwe halitosheki kutazama,
wala sikio halishibi kusikia.
9 [h]Kile kilichokuwepo kitakuwepo
tena,
kile kilichofanyika kitafanyika
tena,
hakuna kilicho kipya chini ya jua.
10 Kuna kitu chochote ambacho mtu
anaweza kusema,
"Tazama! Kitu hiki ni kipya"?
Kilikuwepo tangu zamani za kale,
kilikuwepo kabla ya wakati wetu.
11 [i]Hakuna kumbukumbu ya watu wa
zamani,
hata na wale ambao hawajaja
bado
hawatakumbukwa
na wale watakaofuata baadaye.

*Hekima Ni Ubatili*

12 Mimi, Mhubiri, nilikuwa mfalme wa
Israeli katika Yerusalemu. 13 [j]Nilitumia
muda wangu wote kujifunza na kuvumbua
kwa hekima yote yanayofanyika chini ya
mbingu. Jinsi gani Mungu ameweka mzigo
mzito juu ya wanadamu! 14 [k]Nimeshaona
mambo yote yanayotendeka chini ya jua,
hayo yote ni ubatili, hii ni kukimbiza upepo.

15 [l]Kilichopindika hakiwezi
kunyooshwa,
kile ambacho hakipo haiwezekani
kukihesabu.

16 [m]Niliwaza mwenyewe, "Tazama,
nimekua na kuongezeka katika hekima
kuliko yeyote aliyewahi kutawala
Yerusalemu kabla yangu. Nimekuwa na
uzoefu mkubwa wa hekima na maarifa."
17 [n]Ndipo nilipojitahidi kufahamu
kutofautisha hekima, wazimu na
upumbavu, lakini nikatambua hata hili
nalo ni kukimbiza upepo.

18 [o]Kwa kuwa hekima nyingi huleta
huzuni kubwa;
maarifa yanapoongezeka,
masikitiko yanaongezeka.

---

[a]**1:1** Mhu 7:27; 12:10
[b]**1:2** Za 39:5-6; 62:9; Rum 8:20-21; Mhu 4:4-6; 12:8
[c]**1:3** Mhu 3:9; 5:15-16; 2:11-22
[d]**1:4** 2Pet 3:10; Za 104:5; Ay 8:19
[e]**1:5** Za 19:5-6
[f]**1:7** Ay 36:28; 38:10
[g]**1:8** Mhu 3:1; Mit 27:20
[h]**1:9** Mwa 8:22; Mhu 3:15; 2:12
[i]**1:11** Mhu 8:10; 9:5, 15; 2:16; Za 88:12; Mwa 40:23
[j]**1:13** Mwa 3:17-19; Mhu 3:10; Ay 28:3
[k]**1:14** Mhu 2:11; 4:4; 6:9
[l]**1:15** Mhu 7:13
[m]**1:16** 1Fal 3:12; 4:30; Mhu 2:9
[n]**1:17** 1The 5:21; Mhu 7:23, 25; 2:3, 12; 8:16
[o]**1:18** Mhu 2:23; 12:12; 7:16; Ay 28:28; Yer 45:3

*Anasa Ni Ubatili*

2 [a]Nikafikiri moyoni mwangu, “Haya basi,
nitakujaribu kwa anasa nione ni lipi
lililo jema.” Lakini hilo nalo likaonekana
ni ubatili. 2 [b]Nikasema, “Kicheko nacho ni
upumbavu. Nayo matokeo ya anasa ni nini?”
3 [c]Nikajaribu kujifurahisha kwa mvinyo na
kukumbatia upumbavu, huku bado akili
yangu inaniongoza kwa hekima. Nilitaka
kuona ni lipi bora watu wafanye kwa siku
chache wanazoishi chini ya mbingu.

4 [d]Nikafanya miradi mikubwa:
Nikajijengea majumba na kulima
mashamba ya mizabibu. 5 Nikatengeneza
bustani na viwanja vya starehe nikaotesha
huko kila aina ya miti ya matunda.
6 Nikajenga mabwawa ya kukusanya maji
ya kunyweshea hii miti iliyokuwa inastawi
vizuri. 7 Nikanunua watumwa wa kiume na
wa kike na watumwa wengine walizaliwa
nyumbani mwangu. Pia nilikuwa na
makundi ya ng’ombe, kondoo na mbuzi
kuliko mtu yeyote aliyewahi kuishi
Yerusalemu kabla yangu. 8 [e]Nikajikusanyia
fedha na dhahabu, hazina za wafalme na za
majimbo. Nikajipatia waimbaji wanaume
na wanawake, nazo nyumba za masuria:
vitu ambavyo moyo wa mwanadamu
hufurahia. 9 [f]Nikawa maarufu sana kuliko
mtu mwingine yeyote aliyepata kuishi
Yerusalemu kabla yangu. Katika haya yote
bado nikawa nina hekima.

10 Sikujinyima kitu chochote ambacho
macho yangu yalikitamani,
hakuna anasa ambayo niliunyima
moyo wangu.
Moyo wangu ulifurahia kazi zangu
zote,
hii ilikuwa thawabu ya kazi zangu
zote.

11 Hata hivyo nilipokuja kuangalia yote
ambayo
mikono yangu ilikuwa imefanya
na yale niliyotaabika kukamilisha,
kila kitu kilikuwa ni ubatili, ni
kukimbiza upepo;
hapakuwa na faida yoyote chini ya
jua.

*Hekima Na Upumbavu Ni Ubatili*

12 Kisha nikageuza mawazo yangu
kufikiria hekima,
wazimu na upumbavu.
Ni nini zaidi mtu anayetawala baada
ya mfalme
anachoweza kufanya ambacho
hakijafanywa?
13 [g]Nikaona kuwa hekima ni bora
kuliko upumbavu,
kama vile nuru ilivyo bora kuliko
giza.
14 [h]Mtu mwenye hekima ana macho
katika kichwa chake,
lakini mpumbavu anatembea
gizani;
lakini nikaja kuona kwamba
wote wawili hatima yao
inafanana.

15 [i]Kisha nikafikiri moyoni mwangu,

“Hatima ya mpumbavu itanipata
mimi pia.
Nitafaidi nini basi kwa kuwa na
hekima?”
Nikasema moyoni mwangu,
“Hili nalo ni ubatili.”
16 [j]Kwa maana kwa mtu mwenye
hekima,
kama ilivyo kwa mpumbavu,
hatakumbukwa kwa muda mrefu,
katika siku zijazo wote
watasahaulika.
Kama vile ilivyo kwa mpumbavu,
mtu mwenye hekima pia lazima
atakufa!

[a]**2:1** Za 10:6; Lk 12:19; Mhu 7:4; 8:15
[b]**2:2** Mit 14:13; Isa 22:12-13; Mhu 7:6
[c]**2:3** Amu 9:13; Rut 3:3; Amo 6:3-6; Mhu 3:12-13; 5:18; 8:15
[d]**2:4** 1Fal 7:1-12; Wim 8:11; 2Nya 2:1
[e]**2:8** 1Fal 9:28; 10:10-21; 2Sam 19:35; Amu 3:15
[f]**2:9** 1Nya 29:25; Mhu 1:12-16
[g]**2:13** Mhu 7:11-12, 19; 9:18
[h]**2:14** Za 49:10; Mit 17:24; Mhu 8:1; 3:19; 7:2; 9:3, 11-12
[i]**2:15** Mhu 6:8
[j]**2:16** Za 49:10; 112:6; Mhu 1:11

*Kutaabika Ni Ubatili*

17 Kwa hiyo nikachukia maisha, kwa
sababu kazi inayofanyika chini ya jua
ilikuwa masikitiko kwangu. Yote hayo ni
ubatili, ni kukimbiza upepo. 18 [a]Nikachukia
kila kitu nilichokuwa nimetaabikia chini
ya jua, kwa sababu ni lazima nimwachie
yule ajaye baada yangu. 19 Nani ajuaye
kama atakuwa ni mtu mwenye hekima
au mpumbavu? Lakini hata hivyo yeye
ndiye atakayetawala kazi zote ambazo
nimemiminia juhudi na ustadi chini ya
jua. Hili nalo ni ubatili. 20 Kwa hiyo moyo
wangu ukaanza kukata tamaa juu ya kazi
yangu yote niliyoifanya kwa taabu chini ya
jua. 21 Kwa kuwa mtu anaweza kufanya kazi
yake kwa hekima, maarifa na ustadi, kisha
analazimika kuacha vyote alivyo navyo
kwa mtu mwingine ambaye hajavifanyia
kazi. Hili nalo pia ni ubatili tena ni balaa
kubwa. 22 [b]Mtu atapata nini kwa taabu
yote na kuhangaika kwa bidii katika kazi
anayotaabikia chini ya jua? 23 [c]Siku zake
zote kazi yake ni maumivu na masikitiko,
hata usiku akili yake haipati mapumziko.
Hili nalo pia ni ubatili.

24 [d]Hakuna kitu bora anachoweza kufanya
mtu zaidi ya kula na kunywa na kuridhika
katika kazi yake. Hili nalo pia, ninaona,
latokana na mkono wa Mungu, 25 kwa
sababu pasipo yeye, ni nani awezaye kula na
kufurahi? 26 [e]Kwa yule mtu anayempendeza
Mungu, Mungu humpa hekima, maarifa na
furaha, bali kwa mwenye dhambi Mungu
humpa kazi ya kukusanya na kuhifadhi
utajiri ili Mungu ampe yule anayempenda.
Hili nalo pia ni ubatili, ni kukimbiza upepo.

[a]**2:18** Za 39:6; 49:10; 1Fal 12:13
[b]**2:22** Mhu 3:9; 1:3
[c]**2:23** Ay 5:7; 7:2; 14:1; Mhu 1:18; Mwa 3:17
[d]**2:24** 1Kor 15:32; Mhu 3:12-13, 22; 7:7-10; 8:15; 5:17-19; 9:7-10; 11:7-10; Ay 2:10
[e]**2:26** Ay 27:17; 9:4; Mit 13:22

*Kila Jambo Lina Wakati Wake*

3 [f]Kuna wakati kwa ajili ya kila jambo,
nayo majira kwa kila tendo chini ya mbingu:

2 [g]wakati wa kuzaliwa na wakati wa kufa,
wakati wa kupanda na wakati wa kung'oa yaliyopandwa,
3 [h]wakati wa kuua na wakati wa kuponya,
wakati wa kubomoa,
na wakati wa kujenga,
4 [i]wakati wa kulia na wakati wa kucheka,
wakati wa kuomboleza na wakati wa kucheza,
5 wakati wa kutawanya mawe na wakati wa kukusanya mawe,
wakati wa kukumbatia na wakati wa kutokumbatia,
6 wakati wa kutafuta na wakati wa kupoteza,
wakati wa kuweka na wakati wa kutupa,
7 [j]wakati wa kurarua na wakati wa kushona,
wakati wa kunyamaza na wakati wa kuzungumza,
8 wakati wa kupenda na wakati wa kuchukia,
wakati wa vita na wakati wa amani.

9 Mfanyakazi anapata faida gani kutokana
na taabu yake? 10 [k]Nimeona mzigo Mungu
alioweka juu ya wanadamu. 11 [l]Amefanya
kila kitu kiwe kizuri kwa wakati wake.
Pia ameiweka hiyo milele katika mioyo
ya wanadamu, wala hawawezi kutambua
kwa kina yale ambayo Mungu amefanya
tangu mwanzo hadi mwisho. 12 Ninajua

[f]**3:1** Mhu 8:6
[g]**3:2** Mwa 47:29; Isa 28:24; 38:1
[h]**3:3** Kum 5:17
[i]**3:4** Kut 15:20; 2Sam 6:16
[j]**3:7** Amo 5:13; Es 4:14
[k]**3:10** Mhu 1:13
[l]**3:11** Kum 32:4; Mhu 8:17; Ay 11:7; 28:23; Rum 11:33

kwamba hakuna kitu bora kwa wanadamu
kuliko kuwa na furaha na kutenda mema
wakati wanapoishi. 13 [a]Tena ni karama ya
Mungu kila mtu apate kula na kunywa
na kujiburudisha kwa mema katika kazi
yake yote. 14 [b]Ninajua kwamba kila kitu
anachokifanya Mungu kitadumu milele,
hakuna kinachoweza kuongezwa au
kupunguzwa. Mungu hufanya hivyo ili watu
wamche yeye.

15 [c]Chochote kilichopo kilishakuwepo,
na kitakachokuwepo
kimekwishakuwepo kabla;
naye Mungu huyaita yale
yaliyopita yarudi tena.

16 Pia nikaona kitu kingine tena chini ya
jua:

Mahali pa kutolea hukumu,
uovu ulikuwepo,
mahali pa kupatia haki,
uovu ulikuwepo.

17 [d]Nikafikiri moyoni mwangu,

“Mungu atawaleta hukumuni
wote wawili wenye haki na
waovu,
kwa maana kutakuwako na wakati
kwa ajili ya kila jambo,
wakati kwa ajili ya kila tendo.”

18 [e]Pia nikafikiri, “Kuhusu wanadamu,
Mungu huwajaribu ili wajione kwamba
wao ni kama wanyama. 19 [f]Hatima ya
mwanadamu ni kama ile ya wanyama;
wote wana mwisho unaofanana: Jinsi
anavyokufa mnyama, ndivyo anavyokufa
mwanadamu. Wote wana pumzi
inayofanana; mwanadamu hana cha zaidi
kuliko mnyama. Kila kitu ni ubatili. 20 [g]Wote
huenda mahali panapofanana; wote hutoka
mavumbini, mavumbini wote hurudi. 21 [h]Ni
nani ajuaye kama roho ya mtu huenda juu
na roho ya mnyama hushuka chini ardhini?”
22 [i]Kwa hiyo nikaona kwamba hakuna
kitu kilicho bora zaidi kwa mwanadamu
kuliko kuifurahia kazi yake, kwa sababu
hilo ndilo fungu lake. Kwa maana ni nani
awezaye kumrudisha ili aje kuona kile
kitakachotendeka baada yake?

*Uonevu, Taabu, Uadui*

4 [j]Nikatazama tena nikaona uonevu wote
uliokuwa unafanyika chini ya jua:

Nikaona machozi ya walioonewa,
wala hawana wa kuwafariji;
uwezo ulikuwa upande wa wale
wanaowaonea,
wala hawana wa kuwafariji.
2 [k]Nami nikasema kwamba wafu,
waliokwisha kufa,
wana furaha kuliko watu walio hai,
ambao bado wanaishi.
3 [l]Lakini aliye bora kuliko hao wawili
ni yule ambaye hajazaliwa bado,
ambaye hajaona ule uovu
unaofanyika chini ya jua.

4 Tena nikaona kuwa kazi zote na
mafanikio yote huchipuka kutokana na
wivu wa mtu kwa jirani yake. Hili nalo ni
ubatili, ni kukimbiza upepo.

5 [m]Mpumbavu hukunja mikono yake
na kujiangamiza mwenyewe.
6 [n]Afadhali konzi moja pamoja
na utulivu kuliko konzi mbili
pamoja na taabu
na kukimbiza upepo.

7 Tena nikaona kitu kingine kilicho
ubatili chini ya jua:

[a]**3:13** Za 34:12; Kum 12:7, 18; Mhu 2:3, 24; 5:19
[b]**3:14** Ay 23:15; Yak 1:17; Mhu 5:7; 7:18; 8:12-13
[c]**3:15** Mhu 6:10; 1:9
[d]**3:17** Ay 34:11; 19:29; Mt 16:27; Mhu 11:9; 12:14
[e]**3:18** Za 73:22
[f]**3:19** Mhu 2:14; Za 49:12
[g]**3:20** Mwa 2:7; 3:19-20; Ay 34:10
[h]**3:21** Mhu 12:7
[i]**3:22** Mhu 2:10, 24; 5:18; Ay 31:2
[j]**4:1** Mao 1:16; Mhu 3:16; Za 12:5
[k]**4:2** Mhu 2:17; Yer 20:17-18; 22:10; Ay 3:17; 10
[l]**4:3** Mhu 6:3; Mt 24:19; Ay 3:16-22
[m]**4:5** Mit 6:10
[n]**4:6** Mit 15:16-17; 16:8

[8][a]Kulikuwepo mwanadamu aliye peke
yake,
hakuwa na mwana wala ndugu.
Hapakuwa na mwisho wa kazi yake,
hata hivyo macho yake
hayakutosheka na utajiri wake.
Aliuliza, "Ninajitaabisha hivi kwa
ajili ya nani,
nami kwa nini ninajinyima
kufurahia?"
Hili pia ni ubatili,
ni shughuli yenye taabu!

[9]Wawili ni afadhali kuliko mmoja,
kwa sababu wana malipo mazuri
kwa kazi yao:
[10]Kama mmoja akianguka,
mwenzake atamwinua.
Lakini ni jambo la kuhuzunisha
kwa mtu yule aangukaye
naye hana wa kumwinua!
[11]Pia, kama wawili wakilala pamoja
watapashana joto.
Lakini ni vipi mtu aweza
kujipasha joto mwenyewe?
[12]Ingawa mtu mmoja aweza
kushindwa,
watu wawili wanaweza
kumkabili adui na kumshinda.
Kamba ya nyuzi tatu
haikatiki kwa urahisi.

*Maendeleo Ni Ubatili*

[13] Afadhali kijana maskini mwenye
hekima kuliko mfalme mzee mpumbavu
ambaye hajui tena kupokea maonyo.
[14] Kijana huyo angeweza kutokea gerezani
akapata ufalme, au angeweza kuwa
amezaliwa katika umaskini kwenye huo
ufalme. [15] Nikaona kwamba wote walioishi
na kutembea chini ya jua walimfuata kijana,
aliyepokea ufalme. [16] Hapakuwa na kikomo
cha watu wote aliowatawala. Lakini wale
waliokuja baadaye hawakufurahia kazi ya
yule aliyepokea ufalme. Hili nalo pia ni
ubatili, ni kukimbiza upepo.

[a]**4:8** Mit 27:20; Hab 2:5-6; 1Yn 2:16

*Simama Katika Kicho Cha Mungu*

5 [b]Linda hatua zako uendapo katika
nyumba ya Mungu. Karibia usikilize
kuliko kutoa dhabihu ya wapumbavu,
ambao hawajui kuwa wanafanya kosa.

[2][c]Usiwe mwepesi kuzungumza,
usiwe na haraka katika moyo
wako
kuzungumza lolote mbele za
Mungu.
Mungu yuko mbinguni
nawe uko duniani,
kwa hiyo maneno yako
na yawe machache.
[3][d]Kama vile ndoto huja
wakati kuna shughuli nyingi,
ndivyo yalivyo mazungumzo ya
mpumbavu
wakati kuna maneno mengi.

[4] [e]Wakati unapomwekea Mungu nadhiri,
usikawie kuitimiza. Yeye hafurahii
wapumbavu; timiza nadhiri yako. [5] [f]Ni
afadhali usiweke nadhiri kuliko kuiweka
na usiitimize. [6] Usiruhusu kinywa chako
kukuingiza dhambini. Tena usijitetee mbele
ya huyo mjumbe wa hekaluni, ukisema,
"Niliweka nadhiri kwa makosa." Kwa
nini Mungu akasirike kwa ajili ya yale
unayosema na kuiharibu kazi ya mikono
yako? [7] [g]Kuota ndoto kwingi na maneno
mengi ni ubatili. Kwa hiyo simama katika
kicho cha Mungu.

*Utajiri Ni Ubatili*

[8] [h]Kama ukiona maskini wanaonewa
katika nchi, hukumu na haki vikipotoshwa,
usishangazwe na mambo hayo, kwa maana
afisa mmoja anaangaliwa na aliye juu yake
zaidi na juu ya hao wawili kuna wengine
walio juu zaidi yao. [9] Mafanikio ya nchi ni

[b]**5:1** Za 89:7; Kut 3:5; Hos 6:6
[c]**5:2** Amu 11:35; Ay 6:24; Mit 10:19; 20:25
[d]**5:3** Ay 20:8; Mhu 10:14
[e]**5:4** Mwa 28:20; Kum 23:21; Hes 30:2; Za 76:11; 119:60; Amu 11:35
[f]**5:5** Yon 2:9; Mdo 5:4; Hes 30:2-4
[g]**5:7** Kum 10:12; Mhu 3:14; 12:13
[h]**5:8** Mhu 3:16; 4:1; Za 12:5

kwa ajili ya wote, hata mfalme mwenyewe hufaidi kutoka mashambani.

10 Yeyote apendaye fedha kamwe
hatosheki na fedha;
yeyote apendaye utajiri kamwe
hatosheki na kipato chake.
Hili nalo pia ni ubatili.

11 Mali ikiongezeka, ndivyo walaji
wanavyoongezeka.
Hii nayo inamfaidia nini mwenye
mali
isipokuwa ni kushibisha macho
yake?

12 [a]Usingizi wa kibarua ni mtamu,
awe amekula kidogo au kingi,
lakini wingi wa mali
humnyima tajiri usingizi.

13 [b]Nimeshaona uovu mzito chini ya jua:

Utajiri uliolimbikizwa kwa
kujinyima
na kuleta madhara kwa mwenye
mali,
14 au utajiri uliopotea kwa bahati
mbaya,
hivyo kwamba wakati akiwa na
mwana
hakuna chochote kilichobaki kwa
ajili yake.
15 [c]Mtu hutoka tumboni mwa mama
yake uchi,
naye jinsi alivyokuja vivyo hivyo
huondoka.
Hachukui chochote kutokana na kazi
yake
ambacho anaweza kukibeba
mkononi mwake.

16 [d]Hili nalo ni baya la kusikitisha:

Kama vile mtu ajavyo, vivyo hivyo
huondoka,
naye anapata faida gani,
maadamu hutaabika kwa ajili ya
upepo?

17 Siku zake zote hula gizani,
pamoja na fadhaa kubwa,
mateso na hasira.

18 [e]Ndipo nikatambua kwamba ni vyema
na sahihi kwa mtu kula na kunywa na
kutosheka katika kazi yake ngumu chini
ya jua katika siku chache za maisha yake
Mungu alizompa, kwa maana hili ndilo
fungu lake. 19 [f]Zaidi ya yote, Mungu
anapompa mtu yeyote utajiri na milki,
humwezesha kuvifurahia, kukubali fungu
lake na kuwa na furaha katika kazi yake,
hii ni karama ya Mungu. 20 [g]Mara chache
mtu huzifikiri siku za maisha yake, kwa
sababu Mungu humfanya ashikwe na furaha
ya moyoni.

6 Nimeona ubaya mwingine chini ya
jua, nao unalemea sana wanadamu:
2 [h]Mungu humpa mwanadamu utajiri,
mali na heshima, hivyo hakukosa chochote
moyo wake unachokitamani. Lakini Mungu
hamwezeshi kuvifurahia, badala yake
mgeni ndiye anayevifurahia. Hili ni ubatili,
ni ubaya unaosikitisha.
3 [i]Mtu anaweza kuwa na watoto mia moja
naye akaishi miaka mingi, lakini haidhuru
kuwa ataishi muda mrefu kiasi gani,
kama hawezi kufurahia mafanikio yake
na kwamba hapati mazishi ya heshima,
ninasema afadhali mtoto aliyezaliwa akiwa
amekufa kuliko yeye. 4 Kuzaliwa kwake
hakuna maana, huondokea gizani na gizani
jina lake hufunikwa. 5 Ingawa hakuwahi
kuliona jua wala kujua kitu chochote, yeye
ana pumziko zaidi kuliko mtu huyo, 6 [j]Hata
kama huyo mtu ataishi miaka elfu mara
mbili na zaidi, lakini akashindwa kufurahia
mafanikio yake, je, wote hawaendi sehemu
moja?

---

[a]**5:12** Ay 20:20
[b]**5:13** Mhu 6:1-2
[c]**5:15** Za 49:17; 1Tim 6:7; Ay 1:21; Mhu 1:3
[d]**5:16** Mit 11:29; Mhu 1:3
[e]**5:18** Mhu 2:3, 10, 14, 24
[f]**5:19** 1Nya 29:12; 2Nya 1:12; Ay 31:2; Mhu 2:24; 6:2
[g]**5:20** Kum 12:7, 18; Kut 23:25
[h]**6:2** Kum 8:7-10; Za 17:14; Amu 18:10; Mhu 5:13-19
[i]**6:3** Ay 3:3, 16; Es 7:10; Mhu 4:3
[j]**6:6** Mhu 2:16

7 [a]Juhudi zote za binadamu ni kwa
ajili ya kinywa chake,
hata hivyo hamu yake kamwe
haitoshelezwi.
8 [b]Mtu mwenye hekima ana faida gani
zaidi ya mpumbavu?
Mtu maskini anapata faida gani
kwa kujua jinsi ya kujistahi
mbele ya watu wengine?
9 Ni bora kile ambacho jicho linakiona
kuliko hamu isiyotoshelezwa.
Hili nalo ni ubatili,
ni kukimbiza upepo.

10 [c]Lolote lililopo limekwisha kupewa
jina,
naye mwanadamu alivyo
ameshajulikana;
hakuna mtu awezaye kushindana
na mwenye nguvu kuliko yeye.
11 Maneno yanavyokuwa mengi,
ndivyo yanavyokosa maana,
Je, hilo linamfaidia vipi yeyote?

12 [d]Kwa maana ni nani anayejua lililo
jema kwa ajili ya maisha ya mwanadamu,
katika siku chache na za ubatili anazopita
kama kivuli? Ni nani awezaye kumwambia
yatakayotokea chini ya jua baada ya yeye
kuondoka?

*Hekima*

7 [e]Afadhali sifa nzuri kuliko manukato
safi,
nayo siku ya kufa kuliko ya
kuzaliwa.
2 [f]Afadhali kwenda kwenye nyumba ya
msiba
kuliko kwenda kwenye nyumba ya
karamu,
kwa kuwa kifo ni hatima ya kila
mwanadamu,
imewapasa walio hai kuliweka hili
mioyoni mwao.
3 [g]Huzuni ni afadhali kuliko kicheko,
kwa sababu uso wenye huzuni
wafaa kwa moyo.
4 [h]Moyo wa wenye hekima uko katika
nyumba ya msiba,
lakini moyo wa wapumbavu uko
katika nyumba ya anasa.
5 [i]Afadhali kusikia karipio la mtu
mwenye hekima,
kuliko kusikiliza wimbo wa
wapumbavu.
6 [j]Kama ilivyo kuvunjika kwa miiba
chini ya sufuria,
ndivyo kilivyo kicheko cha
wapumbavu.
Hili nalo pia ni ubatili.

7 [k]Dhuluma humfanya mtu mwenye
hekima kuwa mpumbavu,
nayo rushwa huuharibu moyo.

8 [l]Mwisho wa jambo ni bora kuliko
mwanzo wake,
uvumilivu ni bora kuliko kiburi.
9 [m]Usiwe mwepesi kukasirika rohoni
mwako,
kwa kuwa hasira hukaa kifuani
mwa wapumbavu.

10 Usiseme, "Kwa nini siku za kale
zilikuwa bora kuliko siku
hizi?"
Kwa maana si hekima kuuliza
maswali kama hayo.

11 [n]Hekima, kama ulivyo urithi, ni kitu
chema
na huwafaidia wale walionalo jua.
12 Hekima ni ulinzi kama fedha ilivyo
ulinzi,
lakini faida ya maarifa ni hii:
kwamba hekima huhifadhi maisha
ya aliye nayo.

---

[a]**6:7** Mit 16:26; 27:20; 1Tim 6:6-8
[b]**6:8** Mhu 2:15
[c]**6:10** Ay 9:32; Isa 45:9; Mhu 3:15
[d]**6:12** Yak 4:14; Ay 10:20; 20:8; 14:2; 1Nya 29:15; Za 39:6
[e]**7:1** Ufu 14:13; Wim 1:3; Mit 22:1; Ay 10:18
[f]**7:2** Za 90:12; Mit 11:19; Mhu 2:14
[g]**7:3** 2Kor 7:10; Mit 14:13
[h]**7:4** Mhu 2:1; Yer 16:8
[i]**7:5** Za 141:5; Mit 13:18; 15:31-32
[j]**7:6** Za 58:9; Mhu 2:2; Mit 14:13
[k]**7:7** Kut 18:21; 23:8; Kum 16:19
[l]**7:8** Mit 14:29; Gal 5:22
[m]**7:9** Mit 16:32; 14:17, 29; Mt 5:22
[n]**7:11** Mit 8:10-11; Mhu 2:13; 11:7

13 [a]Tafakari kile Mungu alichokitenda:

Nani awezaye kunyoosha
kile ambacho yeye amekipinda?
14 [b]Nyakati zikiwa nzuri, ufurahi,
lakini nyakati zikiwa mbaya,
tafakari:
Mungu amefanya hiyo moja,
naam, sanjari[c] na hiyo nyingine.
Kwa hiyo, mwanadamu hawezi
kugundua
kitu chochote kuhusu maisha yake
ya baadaye.

15 [d]Katika maisha haya yangu ya ubatili
nimeshaona haya mawili:

mtu mwadilifu akiangamia katika
uadilifu wake,
naye mtu mwovu akiishi maisha
marefu katika uovu wake.
16 Usiwe mwenye haki kupita kiasi,
wala usiwe na hekima kupita
kiasi:
kwa nini kujiangamiza
mwenyewe?
17 [e]Usiwe mwovu kupita kiasi,
wala usiwe mpumbavu:
kwa nini kufa kabla ya wakati
wako?
18 [f]Ni vyema kushika hilo moja
na wala usiache hilo jingine
likupite.
Mtu amchaye Mungu ataepuka
huko kupita kiasi.[g]

19 [h]Hekima humfanya yeye aliye nayo
kuwa na uwezo zaidi
kuliko watawala kumi katika mji.

20 [i]Hakuna mtu mwenye haki duniani
ambaye hufanya mambo ya haki
na kamwe asitende dhambi.

21 [j]Usitie maanani kila neno
linalosemwa na watu,
la sivyo, waweza kumsikia
mtumishi wako akikulaani:
22 kwa kuwa unafahamu moyoni
mwako
kwamba wewe mwenyewe mara
nyingi
umewalaani wengine.

23 [k]Yote haya niliyajaribu kwa hekima,
nikasema,

"Nimeamua kuwa na hekima":
lakini hii ilikuwa nje ya uwezo
wangu.
24 [l]Vyovyote hekima ilivyo,
hekima iko mbali sana na
imejificha,
ni nani awezaye kuigundua?
25 [m]Nikageuza fikira zangu ili kuelewa,
kuchunguza na kuitafuta hekima
na kusudi la mambo,
na ili kuelewa ujinga wa uovu,
na wazimu wa upumbavu.

26 [n]Nimeona jambo lililo chungu kuliko
mauti,
mwanamke ambaye ni mtego,
ambaye moyo wake ni wavu wa
kutegea
na mikono yake ni minyororo.
Mtu ampendezaye Mungu
atamkwepa,
bali mwenye dhambi atanaswa
naye.

27 Mhubiri anasema, "Tazama, hili ndilo
nililogundua:

---

[a]**7:13** Isa 14:27; Mhu 2:24; 1:15
[b]**7:14** Ay 1:21; Mhu 2:24
[c]14 Sanjari hapa maana yake mwandamano wa vitu, wanyama au watu.
[d]**7:15** Mhu 8:14; Yer 12:1; Ay 21:7; 7:7
[e]**7:17** Ay 15:32; Za 55:23
[f]**7:18** Mhu 3:14
[g]18 Au: atafuata hayo yote mawili.
[h]**7:19** Mhu 2:13; 9:13-18; Mit 8:14
[i]**7:20** 1Fal 8:46; Rum 3:12, 23; Gal 3:22; Za 14:3; Mit 20:9; Ay 4:17
[j]**7:21** Mit 30:10
[k]**7:23** Mhu 1:17; Rum 1:22
[l]**7:24** Ay 28:12; 11:12; Isa 55:8-9
[m]**7:25** Ay 28:3; Mhu 1:17
[n]**7:26** Kut 10:7; Amu 14:15; Mit 7:23; 22:14; 2:16-19; 5:3-5

"Nimegundua kitu kimoja baada ya
kingine nilipokuwa katika
kusudi la mambo:
28 [a]ningali natafiti
lakini sipati:
nilimpata mwanaume mmoja
mnyofu miongoni mwa elfu,
lakini hakuna mwanamke mmoja
mnyofu miongoni mwao.
29 Hili ndilo peke yake nililolipata:
Mungu amemuumba mwanadamu
mnyofu,
lakini mwanadamu amebuni
mambo mengi."

8 Ni nani aliye kama mtu mwenye
hekima?
Ni nani ajuaye maelezo ya mambo?
Hekima hung'arisha uso wa mtu
na kubadili ugumu wa uso
wake.

*Mtii Mfalme*

2 Nawaambia, Tii amri ya mfalme,
kwa sababu uliapa mbele za Mungu.
3 [b]Usiharakishe kuondoka mbele ya mfalme.
Usiendelee kutenda lililo baya, kwa maana
mfalme atafanya lolote apendalo. 4 [c]Kwa
kuwa neno la mfalme ndilo lenye mamlaka
ya mwisho, nani awezaye kumwambia, "Je,
wewe unafanya nini?"

5 Yeyote anayetii agizo lake
hatadhurika,
moyo wa hekima utajua wakati
muafaka
na jinsi ya kutenda.
6 [d]Kwa maana kuna wakati muafaka
na utaratibu wa kila jambo,
ingawa huzuni ya mwanadamu
huwa nzito juu yake.
7 Kwa vile hakuna mtu ajuaye siku
zijazo,
ni nani awezaye kumwambia
linalokuja?

8 Hakuna mwanadamu
awezaye kushikilia roho yake
asife,
wala hakuna mwenye uwezo
juu ya siku ya kufa kwake.
Kama vile hakuna yeyote
arudishwaye nyuma wakati
wa vita,
kadhalika uovu hautawaweka
huru wale wautendao.

9 [e]Yote haya niliyaona, nilipokuwa
natafakari kila kitu kinachotendeka chini
ya jua. Kuna wakati ambapo mtu hujifanya
bwana juu ya wengine kwa madhara yake
mwenyewe. 10 Ndipo pia, nikaona waovu
wakizikwa, wale ambao walizoea kuingia
na kutoka mahali patakatifu na kupewa sifa
katika mji ambapo walikuwa wamefanya
haya. Hili nalo ni ubatili.
11 [f]Wakati hukumu juu ya tendo ovu
haitekelezwi upesi, mioyo ya watu hujaa
mipango ya kutenda maovu. 12 [g]Ingawa
mtu mwovu hufanya maovu mia moja na
akaendelea kuishi maisha marefu, najua
kwamba itakuwa bora zaidi kwa watu
wanaomwogopa Mungu, wamchao Mungu.
13 [h]Lakini kwa sababu waovu hawamwogopi
Mungu, hawatafanikiwa, maisha yao
hayatarefuka kama kivuli.
14 [i]Kuna kitu kingine ambacho ni ubatili
kinachotokea duniani: Watu waadilifu
kupata yale yanayowastahili waovu,
nao waovu kupata yale yanayowastahili
waadilifu. Hili nalo pia, nasema ni ubatili.
15 [j]Kwa hiyo mimi ninasifu kufurahia
maisha, kwa sababu hakuna kitu bora
zaidi kwa mwanadamu chini ya jua kuliko
kula, kunywa na kufurahi. Kisha furaha
itafuatana naye kazini mwake siku zote za

[a]**7:28** 1Fal 11:3
[b]**8:3** Rum 13:5; Mhu 10:4
[c]**8:4** Ay 9:12; 34:18; Dan 4:35; Es 1:18-19
[d]**8:6** Mhu 3:1
[e]**8:9** 1Sam 18:12
[f]**8:11** Ay 21:14-15; Rum 2:4-5; Isa 26:10
[g]**8:12** Za 37:18-19; Isa 3:10-11; 65:20; Mhu 3:14; Kum 4:40
[h]**8:13** Mhu 3:14; Kum 4:40; Ay 5:26; Za 34:12; Isa 65:20
[i]**8:14** Za 73:14; Mal 3:15; Mhu 2:14; 7:15; Ay 21:7
[j]**8:15** Law 26:5; Mhu 3:12-13; Kut 32:6; Za 42:8

maisha yake ambazo amepewa na Mungu chini ya jua.
16 [a]Nilipotafakari akilini mwangu ili nijue hekima na kuangalia kazi ya mwanadamu duniani, jinsi ambavyo macho yake hayapati usingizi mchana wala usiku,
17 [b]ndipo nikaona yale yote ambayo Mungu ameyafanya. Hakuna yeyote awezaye kuelewa yale yanayotendeka chini ya jua. Licha ya juhudi zake zote za kutafuta, mtu hawezi kugundua maana yake. Hata ingawa mtu mwenye hekima anadai kuwa anafahamu, kwa hakika hawezi kutambua.

*Hatima Ya Wote*

9 [c]Kwa hiyo niliyatafakari yote haya nikafikia uamuzi kwamba waadilifu na wenye hekima na yale wanayoyafanya yako mikononi mwa Mungu, lakini hakuna mtu ajuaye kama anangojewa na upendo au
chuki. 2 [d]Wote wanayo hatima inayofanana, mwadilifu na mwovu, mwema na mbaya, aliye safi na aliye najisi, wale wanaotoa dhabihu na wale wasiotoa.

Kama ilivyo kwa mtu mwema,
ndivyo ilivyo kwa mtu mwenye dhambi;
kama ilivyo kwa wale wanaoapa,
ndivyo ilivyo kwa wale wasioapa.

3 [e]Huu ni ubaya ulio katika kila kitu kinachotendeka chini ya jua: Mwisho unaofanana huwapata wote. Zaidi ya hayo, mioyo ya watu, imejaa ubaya na kuna wazimu mioyoni mwao wangali hai,
hatimaye huungana na waliokufa. 4 Yeyote aliye miongoni mwa walio hai analo tumaini, hata mbwa hai ni bora kuliko simba aliyekufa!

5 [f]Kwa maana walio hai wanajua kwamba watakufa,
lakini wafu hawajui chochote,
hawana tuzo zaidi,
hata kumbukumbu yao imesahaulika.
6 [g]Upendo wao, chuki yao na wivu wao
vimetoweka tangu kitambo,
kamwe hawatakuwa tena na sehemu
katika lolote linalotendeka chini ya jua.

7 [h]Nenda, kula chakula chako kwa furaha, unywe divai yako kwa moyo wa shangwe, kwa maana sasa Mungu
anakubali unachofanya. 8 [i]Daima uvae nguo nyeupe na daima upake kichwa chako
mafuta. 9 [j]Furahia maisha na mke wako, umpendaye, siku zote za maisha ya ubatili uliyopewa na Mungu chini ya jua, siku zote za ubatili. Kwa maana hili ndilo fungu lako katika maisha na katika kazi yako ya taabu
chini ya jua. 10 [k]Lolote mkono wako upatalo kufanya, fanya kwa nguvu zako zote, kwa kuwa huko kuzimu, unakokwenda, hakuna kufanya kazi wala mipango wala maarifa wala hekima.

11 [l]Nimeona kitu kingine tena chini ya jua:

Si wenye mbio washindao mashindano
au wenye nguvu washindao vita,
wala si wenye hekima wapatao chakula
au wenye akili nyingi wapatao mali,
wala wenye elimu wapatao upendeleo,
lakini fursa huwapata wote.

12 [m]Zaidi ya hayo, hakuna mwanadamu ajuaye wakati saa yake itakapokuja:

---

[a]**8:16** Mhu 1:13-17
[b]**8:17** Ay 5:9; 28:3, 23; Isa 40:28; Rum 11:33
[c]**9:1** Mhu 8:14; 10:14; Kum 33:3; Ay 12:10
[d]**9:2** Ay 9:22; Mhu 2:14; 6:6
[e]**9:3** Mhu 2:14; Yer 11:8; 17:9; Ay 21:26; 9:22; Yer 13:10; 16:12
[f]**9:5** Ay 14:21; Mhu 2:16; Za 9:6; Isa 26:14; 63:16
[g]**9:6** Ay 21:21
[h]**9:7** Mhu 2:24; 8:15; Hes 6:20
[i]**9:8** Za 23:5; Ufu 3:4
[j]**9:9** Mit 5:18; Ay 31:2
[k]**9:10** Isa 38:18; 1Sam 10:7; Rum 12:11; Za 6:5; Mhu 2:24; 11:6; Hes 16:33
[l]**9:11** Amo 2:14-15; Yer 9:23; Kum 8:18; Ay 32:13; Isa 47:10; Mhu 2:14
[m]**9:12** Mit 29:6; Za 73:22; Mhu 8:7; 2:14

Kama vile samaki wavuliwavyo
katika wavu mkatili,
au ndege wanaswavyo kwenye
mtego,
vivyo hivyo wanadamu hunaswa na
nyakati mbaya
zinazowaangukia bila kutazamia.

*Hekima Ni Bora Kuliko Upumbavu*

13 [a]Pia niliona chini ya jua mfano
huu wa hekima ambao ulinivutia sana:
14 Palikuwa na mji mdogo uliokuwa na watu
wachache ndani yake. Mfalme mwenye
nguvu akainuka dhidi yake, akauzunguka
akaweka jeshi kubwa dhidi yake. 15 [b]Katika
mji huo kulikuwepo mtu mmoja maskini
lakini mwenye hekima, naye akauokoa
ule mji kwa hekima yake. Lakini hakuna
aliyemkumbuka yule maskini. 16 [c]Kwa hiyo,
nikasema, "Hekima ni bora kuliko nguvu."
Lakini hekima ya maskini imedharauliwa,
wala hakuna anayesikiliza maneno yake.

17 [d]Maneno ya utulivu ya mwenye
hekima
husikiwa kuliko makelele ya
mtawala wa wapumbavu.
18 [e]Hekima ni bora kuliko silaha za
vita,
lakini mwenye dhambi mmoja
huharibu mema mengi.

10 [f]Kama vile nzi waliokufa huacha
harufu mbaya kwenye
manukato,
ndivyo upumbavu kidogo huzidi
nguvu hekima na heshima.
2 Moyo wa mwenye hekima huelekea
kuume,
lakini moyo wa mpumbavu
huelekea kushoto.
3 Hata anapotembea barabarani,
mpumbavu hukosa ufahamu
na kudhihirisha kwa kila mmoja
jinsi alivyo mpumbavu.

4 [g]Kama hasira ya mtawala ikiwaka
dhidi yako,
usiache mahali pako,
utulivu huweza kuzuia makosa
mengi.

5 Kuna ubaya niliouona chini ya jua,
aina ya kosa litokalo kwa
mtawala:
6 [h]Wapumbavu kuwekwa kwenye
nafasi nyingi za juu,
wakati matajiri hushika nafasi za
chini.
7 [i]Mimi nimeona watumwa
wamepanda farasi,
wakati wakuu wakitembea
kwa miguu kama watumwa.

8 [j]Yeye achimbaye shimo
aweza kutumbukia ndani yake,
yeyote abomoaye ukuta
anaweza kuumwa na nyoka.
9 [k]Yeyote apasuaye mawe
inawezekana yakamuumiza,
yeyote apasuaye magogo
inawezekana yakamuumiza.

10 Kama shoka ni butu
na halikunolewa,
nguvu nyingi zinahitajika,
lakini ustadi utaleta mafanikio.

11 [l]Kama nyoka akiuma kabla ya
kufanyiwa uaguzi,
mwaguzi hatahitajika tena.

12 [m]Maneno yatokayo kinywani mwa
mtu mwenye hekima
yana neema,
bali mpumbavu huangamizwa
na midomo yake mwenyewe.

---

[a]**9:13** 2Sam 20:16-22
[b]**9:15** Mwa 40:14; Mhu 1:11; 2:16
[c]**9:16** Mhu 7:19; Mit 21:22; Es 6:3
[d]**9:17** 2Sam 20:17; Dan 5:10
[e]**9:18** Mhu 2:13; Rum 6:12, 16-23
[f]**10:1** Mit 13:16; 18:2
[g]**10:4** Mit 16:14; 25:15; Mhu 8:3
[h]**10:6** Mit 29:2
[i]**10:7** Mit 19:10
[j]**10:8** Es 2:23; Amo 5:19; Mit 26:27; Za 57:6; 9:16
[k]**10:9** Mit 26:27
[l]**10:11** Yer 8:17; Za 58:5; Isa 3:3
[m]**10:12** Mit 10:14, 32; 14:3; 15:2; 18:7

13 Mwanzoni maneno yake ni
upumbavu,
mwishoni ni wazimu mbaya,
14 [a]naye mpumbavu huzidisha
maneno.

Hakuna yeyote ajuaye linalokuja,
ni nani awezaye kueleza ni jambo
gani
litakalotokea baada yake?

15 Kazi ya mpumbavu humchosha
mwenyewe,
hajui njia iendayo mjini.

16 [b]Ole wako, ee nchi ambayo mfalme
wako alikuwa mtumwa
na ambayo wakuu wako hufanya
karamu asubuhi.
17 [c]Heri wewe, ee nchi ambayo mfalme
wako ni wa uzao wenye
kuheshimika
na ambayo wakuu wako hula
chakula kwa wakati unaofaa:
ili kupata nguvu na si kwa ajili ya
ulevi.

18 [d]Kama mtu ni mvivu paa la nyumba
huinama,
kutokana na mikono milegevu,
nyumba huvuja.

19 [e]Karamu hufanywa kwa ajili ya
kicheko,
nao mvinyo hufurahisha maisha,
lakini fedha ni jawabu la mambo
yote.

20 [f]Usimshutumu mfalme hata ikiwa ni
katika mawazo yako,
au kumlaani tajiri katika chumba
chako cha kulala,
kwa sababu ndege wa angani
wanaweza kuchukua maneno
yako,
naye ndege anayeruka anaweza
kutoa taarifa ya yale
uliyosema.

*Mkate Juu Ya Maji*

11 [g]Tupa mkate wako juu ya maji,
kwa maana baada ya
siku nyingi
utaupata tena.
2 [h]Wape sehemu watu saba, naam hata
wanane,
kwa maana hujui ni baa gani
litakalokuwa juu ya nchi.

3 Kama mawingu yamejaa maji,
hunyesha mvua juu ya nchi.
Kama mti ukianguka kuelekea kusini
au kuelekea kaskazini,
mahali ulipoangukia,
hapo ndipo utakapolala.
4 Yeyote atazamaye upepo hatapanda,
yeyote aangaliaye mawingu
hatavuna.

5 [i]Kama vile usivyofahamu njia ya
upepo,
au jinsi mwili uumbwavyo
ndani ya tumbo la mama,
vivyo hivyo huwezi kufahamu kazi
ya Mungu,
Muumba wa vitu vyote.

6 [j]Panda mbegu yako asubuhi,
nako jioni usiruhusu mikono yako
ilegee,
kwa maana hujui ni ipi
itakayofanikiwa,
kwamba ni hii au ni ile,
au kwamba zote zitafanikiwa
sawasawa.

*Mkumbuke Muumba Wako Ukiwa Bado Kijana*

7 [k]Nuru ni tamu,
tena inafurahisha macho kuona
jua.

---

[a] **10:14** Yak 4:14; Mit 15:2; Mhu 8:7; 5:3; 9:1
[b] **10:16** Isa 3:4-12
[c] **10:17** Mit 31:4; Kum 14:26; 1Sam 25:36
[d] **10:18** Mit 20:4; 24:30-34
[e] **10:19** Mwa 14:18; Amu 9:13
[f] **10:20** Kut 22:28
[g] **11:1** Kum 15:10; 24:19; Hos 10:12; Mt 10:42; Isa 32:20; Mit 19:17
[h] **11:2** Mik 5:5; Efe 5:16; Za 112:9
[i] **11:5** Za 139:14-16; Yn 3:8-10
[j] **11:6** Mhu 9:10
[k] **11:7** Mhu 7:11

8 Hata kama mtu ataishi miaka mingi
kiasi gani,
na aifurahie yote.
Lakini na akumbuke siku za giza,
kwa maana zitakuwa nyingi.
Kila kitu kitakachokuja ni ubatili.

9 [a]Furahi ewe kijana, wakati ungali
kijana,
moyo wako na ukupe furaha
katika siku za ujana wako.
Fuata njia za moyo wako
na chochote macho yako yaonayo,
lakini ujue kwamba kwa ajili ya
haya yote
Mungu atakuleta hukumuni.
10 [b]Kwa hiyo basi, ondoa wasiwasi
moyoni mwako
na utupilie mbali masumbufu ya
mwili wako,
kwa kuwa ujana na nguvu ni
ubatili.

12 [c]Mkumbuke Muumba wako
siku za ujana wako,
kabla hazijaja siku za taabu,
wala haijakaribia miaka
utakaposema,
"Mimi sifurahii hiyo":
2 kabla jua na nuru,
nao mwezi na nyota havijatiwa
giza,
kabla ya kurudi mawingu baada
ya mvua;
3 [d]siku ile walinzi wa nyumba
watakapotetemeka,
nao watu wenye nguvu
watakapojiinamisha,
wakati wasagao watakapokoma kwa
sababu ya uchache,
nao wachunguliao madirishani
kutiwa giza;
4 [e]wakati milango ya kuingia
barabarani itakapofungwa
na sauti ya kusaga kufifia;
wakati watu wataamshwa kwa sauti
ya ndege,
lakini nyimbo zao zote zikififia;
5 [f]wakati watu watakapoogopa
kilichoinuka juu
na hatari zitakazokuwepo
barabarani;
wakati mlozi utakapochanua maua
na panzi kujikokota
nawe usiwe na shauku ya kitu
chochote.
Ndipo mwanadamu aiendea nyumba
yake ya milele
nao waombolezaji wakizunguka
barabarani.

6 Mkumbuke Muumba wako: kabla
haijakatika kamba ya fedha,
au bakuli la dhahabu
halijavunjika;
kabla mtungi kuvunjika kwenye
chemchemi,
au gurudumu kuvunjika kisimani,
7 [g]nayo mavumbi kurudi ardhini
yalikotoka,
na roho kurudi kwa Mungu
aliyeitoa.

8 Mhubiri asema, "Ubatili! Ubatili!
Kila kitu ni ubatili!"

*Hitimisho La Mambo*

9 [h]Mhubiri hakuwa tu na hekima, bali
aliwagawia watu maarifa pia. Alitafakari
na kutafiti na akaweka katika utaratibu
mithali nyingi. 10 [i]Mhubiri alitafiti ili
kupata maneno sahihi na kila alichoandika
kilikuwa sawa na kweli.
11 [j]Maneno ya wenye hekima ni kama
mchokoro, mithali zao zilizokusanywa
pamoja ni kama misumari iliyogongomewa
ikawa imara, yaliyotolewa na Mchungaji
mmoja. 12 Tena zaidi ya hayo, mwanangu,
kubali maonyo, hakuna mwisho wa kutunga

[a] **11:9** Ay 19:29; Kum 29:19; Mdo 14:16; Rum 14:10; Mhu 2:24; 3:17
[b] **11:10** 2Kor 7:1; Za 94:19; Mhu 2:24
[c] **12:1** 2Sam 19:35; Mhu 11:8
[d] **12:3** Mwa 27:1; Zek 8:4; Za 71:9
[e] **12:4** Yer 25:10; Mik 7:1
[f] **12:5** Ay 10:21; 17:13; Yer 9:17; Amo 5:16
[g] **12:7** Mwa 2:7; Ay 20:8; 34:15; Mhu 3:21; Za 146:4
[h] **12:9** 1Fal 4:32
[i] **12:10** Mit 22:20-21
[j] **12:11** Ezr 9:8; Ay 6:25

vitabu vingi, nako kusoma sana huuchosha
mwili.

13 [a]Hii ndiyo jumla ya maneno;
yote yamekwisha sikiwa:
Mche Mungu, nawe uzishike amri
zake,
maana kwa jumla ndiyo impasayo
mtu.
14 [b]Kwa maana Mungu ataleta
hukumuni kila kazi,
pamoja na kila neno la siri,
likiwa jema au baya.

---

[a] **12:13** Mik 6:8; Kum 4:2-6; 10:12; Kut 20:20; 1Sam 12:24; Ay 23:15; Za 19:9
[b] **12:14** Mt 10:26; Ay 19:26; 34:21; Mhu 3:17; Za 19:12; Yer 16:17

# WIMBO ULIO BORA

1 [a]Wimbo ulio bora wa Solomoni.

*Shairi La Kwanza*

*Mpendwa*

2 [b]Unibusu kwa busu la kinywa chako,
kwa maana upendo wako
unafurahisha kuliko divai.
3 [c]Manukato yako yananukia vizuri,
jina lako ni kama manukato
yaliyomiminwa.
Ndiyo sababu wanawali
wanakupenda!
4 [d]Nichukue twende nawe, na tufanye
haraka!
Mfalme na anilete ndani ya vyumba
vyake.

*Marafiki*

Tunakushangilia na kukufurahia,
tutasifu upendo wako zaidi kuliko
divai.

*Mpendwa*

Tazama jinsi ilivyo bora wakupende!
5 [e]Mimi ni mweusi, lakini napendeza,
enyi binti za Yerusalemu,
mweusi kama mahema ya Kedari,
kama mapazia ya hema la
Solomoni.
6 [f]Usinikazie macho kwa sababu mimi
ni mweusi,
kwa sababu nimefanywa mweusi
na jua.
Wana wa mama yangu
walinikasirikia
na kunifanya niwe mtunza
mashamba ya mizabibu.
Shamba langu mwenyewe la
mizabibu nimeliacha.

7 [g]Niambie, wewe ambaye
ninakupenda,
unalisha wapi kundi lako la
kondoo
na ni wapi unapowapumzisha
kondoo wako adhuhuri.
Kwa nini niwe kama mwanamke
aliyefunikwa shela
karibu na makundi ya rafiki zako?

*Marafiki*

8 [h]Kama hujui, ewe mwanamke mzuri
kuliko wote,
fuata nyayo za kondoo,
na kulisha wana-mbuzi wako
karibu na hema za wachungaji.

*Mpenzi*

9 [i]Mpenzi wangu, ninakufananisha na
farasi jike
aliyefungwa katika mojawapo ya
magari ya vita ya Farao.
10 [j]Mashavu yako yanapendeza yakiwa
na vipuli,
shingo yako ikiwa na mikufu ya
vito.
11 Tutakufanyia vipuli vya dhahabu,
vyenye kupambwa kwa fedha.

*Mpendwa*

12 [k]Wakati mfalme alipokuwa mezani
pake,
manukato yangu yalisambaza
harufu yake nzuri.
13 [l]Mpenzi wangu kwangu mimi ni
kifuko cha manemane
kati ya matiti yangu.
14 [m][n]Mpenzi wangu kwangu mimi ni

[a]**1:1** 1Fal 4:32; Za 45
[b]**1:2** Wim 8:6; Mwa 14:18; Amu 9:13; Wim 4:10
[c]**1:3** Es 2:12; Za 45:8-14; Mhu 7:1
[d]**1:4** Yer 31:3; Flp 3:12; Wim 2:3
[e]**1:5** Wim 2:14; 2:7; 5:16; 4:3; Mwa 25:13
[f]**1:6** Za 69:8; Wim 7:12; 8:12; 2:15
[g]**1:7** Wim 3:1-4; Isa 13:20; Mwa 24:65
[h]**1:8** Wim 5:9; 6:1
[i]**1:9** Wim 2:2; 2Nya 1:16-17
[j]**1:10** Eze 16:11; Isa 61:10; Wim 5:13
[k]**1:12** Wim 4:11-14
[l]**1:13** Mwa 37:25
[m]**1:14** Wim 4:13; 1Sam 23:29
[n]**1:14** 2Nya 20:2; Wim 2:3; 5:8

kama kishada cha maua ya mhina
kutoka mashamba ya mizabibu ya En-Gedi.

*Mpenzi*

15 [a]Tazama jinsi ulivyo mzuri, mpenzi wangu!
Tazama jinsi ulivyo mzuri!
Macho yako ni kama ya hua.

*Mpendwa*

16 Tazama jinsi ulivyo mzuri, mpenzi wangu!
Ee, tazama jinsi unavyopendeza!
Na kitanda chetu ni cha majani mazuri.

*Mpenzi*

17 [b]Nguzo za nyumba yetu ni mierezi,
na mapao yetu ni miberoshi.

*Mpendwa*

2 1 [c]Mimi ni ua la Sharoni,
yungiyungi ya bondeni.

*Mpenzi*

2 Kama yungiyungi katikati ya miiba
ndivyo alivyo mpenzi wangu
katikati ya wanawali.

*Mpendwa*

3 [d]Kama mti wa mtofaa miongoni mwa miti ya msituni
ndivyo alivyo mpenzi wangu
miongoni mwa wanaume vijana.
Ninafurahia kuketi kivulini mwa mwanaume huyu,
na tunda lake ni tamu kwangu.
4 [e]Amenichukua mpaka kwenye ukumbi wa karamu,
na bendera ya huyu mwanaume
juu yangu ni upendo.
5 [f]Nitie nguvu kwa zabibu kavu,
niburudishe kwa matofaa,
kwa maana ninazimia kwa mapenzi.
6 [g]Mkono wake wa kushoto uko chini ya kichwa changu,
na mkono wake wa kuume unanikumbatia.
7 [h]Binti za Yerusalemu, ninawaagiza
kwa paa na kwa ayala wa shambani:
Msichochee wala kuamsha mapenzi
hata yatakapotaka yenyewe.

*Shairi La Pili*

*Mpendwa*

8 [i]Sikiliza! Mpenzi wangu!
Tazama! Huyu hapa anakuja,
akirukaruka juu milimani
akizunguka juu ya vilima.
9 [j]Mpenzi wangu ni kama paa au ayala kijana.
Tazama! Anasimama nyuma ya ukuta wetu,
akitazama kupitia madirishani,
akichungulia kimiani.
10 Mpenzi wangu alizungumza na kuniambia,
"Inuka, mpenzi wangu,
mrembo wangu, tufuatane.
11 Tazama! Wakati wa masika umepita,
mvua imekwisha na ikapita.
12 Maua yanatokea juu ya nchi;
majira ya kuimba yamewadia,
sauti za njiwa zinasikika
katika nchi yetu.
13 [kl]Mtini unatunga matunda yake ya mwanzoni,
zabibu zinazochanua zaeneza harufu nzuri.
Inuka, njoo mpenzi wangu.
Mrembo wangu, tufuatane."

---

[a]**1:15** Wim 4:7; 7:6; Za 74:19; Yer 48:28
[b]**1:17** 1Fal 6:9
[c]**2:1** 1Nya 27:29; Hos 14:5; Wim 5:13; Isa 55:1
[d]**2:3** Mwa 3:6; Wim 1:4, 14; 4:16
[e]**2:4** Es 1:11; Hes 1:52
[f]**2:5** Wim 7:8; 5:8
[g]**2:6** Wim 8:3
[h]**2:7** Wim 5:8; 3:5; 8:4
[i]**2:8** Wim 8:14
[j]**2:9** 2Sam 2:18; Wim 8:14
[k]**2:13** Nah 3:12; Wim 7:12
[l]**2:13** Mik 7:1; Isa 28:4; Yer 24:2; Hos 9:10

*Mpenzi*

[14] [a]Hua wangu penye nyufa za majabali,
mafichoni pembezoni mwa mlima,
nionyeshe uso wako,
na niisikie sauti yako,
kwa maana sauti yako ni tamu,
na uso wako unapendeza.
[15] [b]Tukamatie mbweha,
mbweha wale wadogo
wanaoharibu mashamba ya mizabibu,
mashamba yetu ya mizabibu yaliyochanua.

*Mpendwa*

[16] [c]Mpenzi wangu ni wangu, nami ni wake,
yeye hujilisha katikati ya yungiyungi.
[17] [d]Mpaka jua linapochomoza,
na vivuli vikimbie,
rudi, mpenzi wangu,
na uwe kama paa,
au kama ayala kijana
juu ya vilima vya Betheri.

3 [e]Usiku kucha kwenye kitanda changu
nilimtafuta yule moyo wangu umpendaye;
nilimtafuta, lakini sikumpata.
[2] Sasa nitaondoka na kuzunguka mjini,
katika barabara zake na viwanja;
nitamtafuta yule moyo wangu umpendaye.
Kwa hiyo nilimtafuta lakini sikumpata.
[3] [f]Walinzi walinikuta
walipokuwa wakizunguka mji.
Nikawauliza, “Je, mmemwona
yule moyo wangu umpendaye?”
[4] [g]Kitambo kidogo tu baada ya kuwapita
nilimpata yule moyo wangu umpendaye.
Nilimshika na sikumwachia aende
mpaka nilipomleta katika nyumba ya mama yangu,
katika chumba cha yule aliyenichukua mimba.
[5] [h]Binti za Yerusalemu, ninawaagiza
kwa paa na kwa ayala wa shambani:
Msichochee wala kuamsha mapenzi
hata yatakapotaka yenyewe.

*Shairi La Tatu*

*Mpenzi*

[6] [i]Ni nani huyu anayekuja kutoka jangwani
kama nguzo ya moshi,
anayenukia manemane na uvumba
iliyotengenezwa kwa vikolezo vyote
vya mfanyabiashara?
[7] [j]Tazama! Ni gari la Solomoni
lisindikizwalo na mashujaa sitini,
walio wakuu sana wa Israeli,
[8] [k]wote wamevaa panga,
wote wazoefu katika vita,
kila mmoja na upanga wake pajani,
wamejiandaa kwa ajili ya hofu za usiku.
[9] Mfalme Solomoni alijitengenezea gari;
alilitengeneza kwa mbao kutoka Lebanoni.
[10] [l]Nguzo zake alizitengeneza kwa fedha,
kitako chake kwa dhahabu.

---

[a]**2:14** Wim 8:13; Mwa 8:8; Wim 1:15
[b]**2:15** Amu 15:4; Wim 7:12; Eze 13:4; Za 80:13
[c]**2:16** Wim 7:10; 4:5; 6:3
[d]**2:17** Wim 4:6; 1:14; Rum 13:12
[e]**3:1** Isa 26:9; Wim 5:6
[f]**3:3** Wim 5:7; Isa 21:6-11
[g]**3:4** Wim 8:2; 6:9; 8:5; Rum 8:35-39; Mit 8:17; 4:13
[h]**3:5** Wim 2:7; 8:4
[i]**3:6** Wim 8:6; 4:6, 14; Kut 30:34; Yer 2:2
[j]**3:7** 1Sam 8:11
[k]**3:8** Ay 15:22; Za 91:5
[l]**3:10** Mt 22:37; Efe 3:19; Rum 5:8

Kiti chake kilipambwa kwa zambarau,
gari lake likanakshiwa njumu kwa upendo
na binti za Yerusalemu.
11 [a]Tokeni nje, ninyi binti za Sayuni,
mkamtazame Mfalme Solomoni akiwa amevaa taji,
taji ambalo mama yake alimvika
siku ya arusi yake,
siku ambayo moyo wake ulishangilia.

*Mpenzi*

4 1 [b]Tazama jinsi ulivyo mzuri, mpenzi wangu!
Ee, jinsi ulivyo mzuri!
Macho yako nyuma ya shela yako
ni kama ya hua.
Nywele zako ni kama kundi la mbuzi
zikishuka kutoka Mlima Gileadi.
2 [c]Meno yako ni kama kundi la kondoo
waliokatwa manyoya sasa hivi,
watokao kuogeshwa.
Kila mmoja ana pacha lake,
hakuna hata mmoja aliye peke yake.
3 [d]Midomo yako ni kama uzi mwekundu,
kinywa chako kinapendeza.
Mashavu yako nyuma ya shela yako
ni kama vipande viwili vya komamanga.
4 [e]Shingo yako ni kama mnara wa Daudi,
uliojengwa kwa madaha,
juu yake zimetundikwa ngao elfu,
zote ni ngao za mashujaa.
5 [f]Matiti yako mawili ni kama wana-paa wawili,
kama wana-paa mapacha
wajilishao katikati ya yungiyungi.
6 [g]Hata kupambazuke na vivuli vikimbie,
nitakwenda kwenye mlima wa manemane
na kwenye kilima cha uvumba.
7 [h]Wewe ni mzuri kote, mpenzi wangu,
hakuna hitilafu ndani yako.

8 [i]Enda nami kutoka Lebanoni, bibi arusi wangu,
enda nami kutoka Lebanoni.
Shuka kutoka ncha ya Amana,
kutoka juu ya Seniri, kilele cha Hermoni,
kutoka mapango ya simba
na kutoka mlima wapendapo kukaa chui.
9 [j]Umeiba moyo wangu, dada yangu, bibi arusi wangu;
umeiba moyo wangu
kwa mtazamo mmoja wa macho yako,
kwa kito kimoja cha mkufu wako.
10 [k]Tazama jinsi pendo lako linavyofurahisha,
dada yangu, bibi arusi wangu!
Pendo lako linafurahisha aje zaidi ya divai,
na harufu ya manukato yako zaidi ya kikolezo chochote!
11 [l]Midomo yako inadondosha utamu kama sega la asali,
bibi arusi wangu;
maziwa na asali viko chini ya ulimi wako.
Harufu nzuri ya mavazi yako ni kama ile ya Lebanoni.
12 [m]Wewe ni bustani iliyofungwa, dada yangu,
bibi arusi wangu;

[a]**3:11** Isa 3:16; 54:5; 32:9-13; 62:5; Yer 3:14
[b]**4:1** Wim 1:15; 5:12; Mwa 37:25; Hes 32:1; Mwa 24:65; Yer 22:6; Mik 7:14
[c]**4:2** Wim 6:6
[d]**4:3** Wim 5:16; 6:7
[e]**4:4** Eze 27:10; Neh 3:19; 2Sam 22:51; Za 144:12
[f]**4:5** Wim 7:3; 6:2-3; Mit 5:19; Isa 66:10-12
[g]**4:6** Wim 2:6-7; 3:6; 2:17
[h]**4:7** Wim 1:15
[i]**4:8** Kum 3:9; 1Nya 5:23; Wim 5:1
[j]**4:9** Isa 54:5; Za 73:6; Yn 3:29; Mwa 41:43
[k]**4:10** Wim 7:6; 1:2; Amu 9:13; Za 45:8; Isa 57:9
[l]**4:11** Hos 14:6; Za 19:10; Mit 24:13-14; Mwa 27:27
[m]**4:12** Mit 5:15-18; Isa 58:11; Wim 6:2; 5:1

wewe ni chanzo cha maji
kilichozungushiwa kabisa,
chemchemi yangu peke yangu.
13 [a]Mimea yako ni bustani ya
mikomamanga
yenye matunda mazuri sana,
yenye hina na nardo,
14 [b]nardo na zafarani,
mchai na mdalasini,
pamoja na kila aina ya mti wa
uvumba,
manemane na udi,
na aina zote za vikolezo bora
kuliko vyote.
15 [c]Wewe ni chemchemi ya bustani,
kisima cha maji yatiririkayo,
yakitiririka kutoka Lebanoni.

*Mpendwa*

16 [d]Amka, upepo wa kaskazini,
na uje, upepo wa kusini!
Vuma juu ya bustani yangu,
ili harufu yake nzuri iweze kuenea
mpaka ng'ambo.
Mpendwa wangu na aje bustanini
mwake
na kuonja matunda mazuri sana.

*Mpenzi*

5 1 [e]Nimekuja kwenye bustani yangu,
dada yangu,
bibi arusi wangu;
nimekusanya manemane yangu
pamoja
na kikolezo changu.
Nimekula sega langu la asali na asali
yangu;
nimekunywa divai yangu na
maziwa yangu.

*Marafiki*

Kuleni, enyi marafiki, mnywe;
kunyweni ya kutosha, ee wapenzi.

*Shairi La Nne*

*Mpendwa*

2 [f][g]Nililala lakini moyo wangu
ulikuwa macho.
Sikiliza! Mpenzi wangu anabisha:
"Nifungulie, dada yangu, mpenzi
wangu,
hua wangu, asiye na hitilafu.
Kichwa changu kimeloa umande,
na nywele zangu manyunyu ya
usiku."
3 Nimevua joho langu:
je, ni lazima nivae tena?
Nimenawa miguu yangu:
je, ni lazima niichafue tena?
4 Mpenzi wangu aliweka mkono wake
kwenye tundu la komeo;
moyo wangu ulianza kugonga kwa
ajili yake.
5 Niliinuka kumfungulia mpenzi
wangu,
mikono yangu ikidondosha
manemane,
vidole vyangu vikitiririka
manemane,
penye vipini vya komeo.
6 [h][i]Nilimfungulia mpenzi wangu,
lakini mpenzi wangu
alishaondoka;
alikuwa amekwenda zake.
Moyo wangu ulishuka kwa kuondoka
kwake.
Nilimtafuta lakini sikumpata.
Nilimwita lakini hakunijibu.
7 [j]Walinzi walinikuta
walipokuwa wakifanya zamu za
ulinzi mjini.
Walinipiga, wakanijeruhi,
wakaninyang'anya joho langu,
hao walinzi wa kuta!
8 [k]Enyi binti za Yerusalemu,
ninawaagiza:
kama mkimpata mpenzi wangu,

---

[a]**4:13** Wim 6:11; 7:12; 1:14
[b]**4:14** Kut 30:23; Wim 3:6; 1:12; Hes 24:6
[c]**4:15** Isa 27:2; 58:11; Yer 31:12; Mit 5:18
[d]**4:16** Wim 2:3
[e]**5:1** Yoe 3:18; Wim 4:12; 4:16; Isa 55:1
[f]**5:2** Efe 5:27
[g]**5:2** Mit 8:4; Wim 6:9; 4:7; 1:15
[h]**5:6** Wim 6:1-2; 3:1
[i]**5:6** Hos 5:15; Mao 3:8
[j]**5:7** Wim 3:3
[k]**5:8** Wim 2:7; 1:14; 2:5

mtamwambia nini?
Mwambieni ninazimia kwa
mapenzi.

*Marafiki*

9 Je, mpendwa wako ni bora kuliko
wengine namna gani,
wewe uliye mzuri kupita
wanawake wote?
Je, mpendwa wako ni mzuri kuliko
wengine, namna gani,
hata unatuagiza hivyo?

*Mpendwa*

10 [a]Mpenzi wangu anang'aa, tena ni
mwekundu,
wa kuvutia miongoni mwa
wanaume kumi elfu.
11 Kichwa chake ni dhahabu safi kuliko
zote,
nywele zake ni za mawimbi
na ni nyeusi kama kunguru.
12 [b]Macho yake ni kama ya hua
kandokando ya vijito vya maji,
aliyeogeshwa kwenye maziwa,
yaliyopangwa kama vito vya
thamani.
13 Mashavu yake ni kama matuta ya
vikolezo
yakitoa manukato.
Midomo yake ni kama yungiyungi
inayodondosha manemane.
14 [c]Mikono yake ni fimbo za dhahabu
iliyopambwa kwa krisolitho.
Mwili wake ni kama pembe ya
ndovu iliyong'arishwa
iliyopambwa na yakuti samawi.
15 [d]Miguu yake ni nguzo za marmar
zilizosimikwa katika vitako vya
dhahabu safi.
Sura yake ni kama Lebanoni,
bora kama miti yake ya mierezi.
16 [e]Kinywa chake chenyewe ni utamu,
kwa ujumla yeye ni wa
kupendeza.
Huyu ndiye mpenzi wangu, huyu
ndiye rafiki yangu,
ee binti za Yerusalemu.

*Marafiki*

6 1 [f]Mpenzi wako amekwenda wapi,
ewe mzuri kupita wanawake
wote?
Mpenzi wako amegeukia njia ipi,
tupate kumtafuta pamoja nawe?

*Mpendwa*

2 [g]Mpenzi wangu amekwenda
bustanini mwake,
kwenye vitalu vya vikolezo,
kujilisha bustanini
na kukusanya yungiyungi.
3 [h]Mimi ni wake mpenzi wangu,
na mpenzi wangu ni wangu;
yeye hujilisha katikati ya
yungiyungi.

*Shairi La Tano*

*Mpenzi*

4 [i]Wewe ni mzuri, mpenzi wangu,
kama Tirsa,
upendezaye kama Yerusalemu,
umetukuka kama jeshi lenye
bendera.
5 Uyageuze macho yako mbali nami,
yananigharikisha.
Nywele zako ni kama kundi la mbuzi
wanaoteremka kutoka Gileadi.
6 Meno yako ni kama kundi la kondoo
watokao kuogeshwa.
Kila mmoja ana pacha lake,
hakuna hata mmoja aliye peke
yake.
7 [j]Mashavu yako nyuma ya shela yako
ni kama vipande viwili vya
komamanga.
8 [k]Panaweza kuwepo malkia sitini,
masuria themanini
na mabikira wasiohesabika;

---

[a] **5:10** Za 45:2
[b] **5:12** Mwa 49:12; Wim 1:15
[c] **5:14** Ay 28:6
[d] **5:15** 1Fal 4:33; Wim 7:4
[e] **5:16** Wim 4:3; 7:9; Yer 31:3; Rum 8:35
[f] **6:1** Wim 1:8; 5:6
[g] **6:2** Sef 3:17; Isa 40:11; Wim 4:12; 5:13; 5:6
[h] **6:3** Wim 7:10; 2:16
[i] **6:4** 2Kor 10:4; 1Fal 15:33; Yos 12; 24; Za 48:2; Hes 1:52; Za 50:2
[j] **6:7** Mwa 24:65; Wim 4:3
[k] **6:8** Za 45:9; Mwa 22:24; Es 2:14

9 [a]lakini hua wangu, mkamilifu
wangu,
ni wa namna ya pekee,
binti pekee kwa mama yake,
kipenzi cha yeye aliyemzaa.
Wanawali walimwona na kumwita
aliyebarikiwa;
malkia na masuria walimsifu.

*Marafiki*

10 Ni nani huyu atokeaye kama
mapambazuko,
mzuri kama mwezi, mwangavu
kama jua,
ametukuka kama nyota
zifuatanazo?

*Mpenzi*

11 [b]Niliteremka kwenye bustani ya miti
ya milozi
ili kutazama machipuko ya
bondeni,
kuona kama mizabibu imechipua
au kama mikomamanga
imechanua maua.
12 Kabla sijang'amua,
shauku yangu iliniweka
katikati ya magari ya kifalme ya
kukokotwa na farasi ya watu
wangu.

*Marafiki*

13 [c]Rudi, rudi, ee Mshulami;
rudi, rudi ili tupate kukutazama!

*Mpenzi*

Kwa nini kumtazama Mshulami,
kama kutazama ngoma ya
Mahanaimu?[d]

7 [e]Ee binti wa mwana wa mfalme,
tazama jinsi inavyopendeza
miguu yako katika viatu!
Miguu yako yenye madaha ni kama
vito vya thamani,
kazi ya mikono ya fundi stadi.
2 Kitovu chako ni kama bilauri ya
mviringo
ambayo kamwe haikosi divai
iliyochanganywa.
Kiuno chako ni kichuguu cha ngano
kilichozungukwa kwa yungiyungi.
3 [f]Matiti yako ni kama wana-paa
wawili,
mapacha wa paa.
4 [g]Shingo yako ni kama mnara wa
pembe ya ndovu.
Macho yako ni vidimbwi vya
Heshboni
karibu na lango la Beth-Rabi.
Pua lako ni kama mnara wa
Lebanoni
ukitazama kuelekea Dameski.
5 [h]Kichwa chako kinakuvika taji kama
mlima Karmeli.
Nywele zako ni kama zulia la
urujuani;
mfalme ametekwa na mashungi
yake.
6 [i]Tazama jinsi ulivyo mzuri na
unavyopendeza,
ee pendo, kwa uzuri wako!
7 [j]Umbo lako ni kama la mtende,
nayo matiti yako kama vishada
vya matunda.
8 [k]Nilisema, "Nitakwea mtende,
nami nitayashika matunda yake."
Matiti yako na yawe kama vishada
vya mzabibu,
harufu nzuri ya pumzi yako kama
matofaa,
9 [l]na kinywa chako kama divai
bora kuliko zote.

*Mpendwa*

Divai na iende moja kwa moja hadi
kwa mpenzi wangu,
ikitiririka polepole juu ya midomo
na meno.

---

[a]**6:9** Wim 1:15; 5:2; 3:4
[b]**6:11** Wim 7:12
[c]**6:13** Kut 15:20
[d]13 Mahanaimu hapa ina maana ya majeshi mawili.
[e]**7:1** Za 45:13
[f]**7:3** Wim 4:5
[g]**7:4** Hes 21:26; Wim 4:4; 5:15; Za 144:12
[h]**7:5** Isa 35:2
[i]**7:6** Wim 1:15; 4:10
[j]**7:7** Wim 4:5
[k]**7:8** Wim 2:5
[l]**7:9** Wim 5:16

10 [a]Mimi ni mali ya mpenzi wangu,
nayo shauku yake ni juu yangu.
11 Njoo, mpenzi wangu, twende mashambani,
twende tukalale huko vijijini.
12 [b]Hebu na twende mapema
katika mashamba ya mizabibu
tuone kama mizabibu imechipua,
kama maua yake yamefunguka,
na kama mikomamanga imetoa maua:
huko nitakupa penzi langu.
13 [cd]Mitunguja hutoa harufu zake nzuri,
kwenye milango yetu kuna matunda mazuri,
mapya na ya zamani,
ambayo nimekuhifadhia wewe,
mpenzi wangu.

8 [e]Laiti ungelikuwa kwangu kama ndugu wa kiume,
ambaye aliyanyonya matiti ya mama yangu!
Kisha, kama ningekukuta huko nje,
ningelikubusu,
wala hakuna mtu yeyote angelinidharau.
2 Ningelikuongoza na kukuleta
katika nyumba ya mama yangu,
yeye ambaye amenifundisha.
Ningelikupa divai iliyokolezwa unywe,
asali ya maua ya mikomamanga yangu.
3 [f]Mkono wake wa kushoto uko chini ya kichwa changu,
na mkono wake wa kuume unanikumbatia.
4 [g]Binti za Yerusalemu, ninawaagiza:
msichochee wala kuamsha mapenzi
hata yatakapotaka yenyewe.

*Shairi La Sita*

*Marafiki*

5 [h]Ni nani huyu anayekuja kutoka nyikani
akimwegemea mpenzi wake?

*Mpendwa*

Nilikuamsha chini ya mtofaa,
huko mama yako alipotunga mimba yako,
huko yeye alipata utungu akakuzaa.
6 [i]Nitie kama muhuri moyoni mwako,
kama muhuri kwenye mkono wako;
kwa maana upendo una nguvu kama mauti,
wivu wake ni mkatili kama kuzimu.
Unachoma kama mwali wa moto,
kama mwali mkubwa wa moto wa BWANA hasa.
7 [j]Maji mengi hayawezi kuuzimisha upendo,
mito haiwezi kuugharikisha.
Kama mtu angelitoa mali yote ya nyumbani mwake
kwa ajili ya upendo,
angelidharauliwa kabisa.

*Marafiki*

8 Tunaye dada mdogo,
matiti yake hayajakua bado.
Tutafanya nini kwa ajili ya dada yetu
wakati atakapokuja kuposwa?
9 Kama yeye ni ukuta,
tutajenga minara ya fedha juu yake.
Na kama yeye ni mlango,
tutamzungushia mbao za mierezi.

*Mpendwa*

10 [k]Mimi ni ukuta,
nayo matiti yangu ni kama minara.

---

[a]**7:10** Wim 2:16; 6:3; Za 45:11; Gal 2:20
[b]**7:12** Za 63:3-8; Wim 6:11; 4:13; 2:13-15
[c]**7:13** Gal 5:22
[d]**7:13** Mwa 30:14; Wim 4:16
[e]**8:1** Mit 9:2; Wim 3:4
[f]**8:3** Wim 2:6
[g]**8:4** Wim 2:7; 3:5
[h]**8:5** Wim 3:4-6; Yn 17:14
[i]**8:6** Wim 1:2; Hes 5:14; Hag 2:23; Isa 49:16
[j]**8:7** Mit 6:35
[k]**8:10** Kol 2:7; Eze 16:7

Ndivyo ambavyo nimekuwa machoni
pake
kama yule anayeleta utoshelevu.
11 [a]Solomoni alikuwa na shamba la
mizabibu huko Baal-Hamoni;
alikodisha shamba lake la
mizabibu kwa wapangaji.
Kila mmoja angeleta kwa ajili ya
matunda yake
shekeli 1,000[b] za fedha.
12 Lakini shamba langu la mizabibu
ambalo ni langu mwenyewe
ni langu kutoa;
hizo shekeli 1,000 ni kwa ajili yako,
ee Solomoni,
na shekeli mia mbili[c] ni kwa ajili
ya wale wanaotunza matunda
yake.

*Mpenzi*

13 [d]Wewe ukaaye bustanini
pamoja na marafiki mliohudhuria,
hebu nisikie sauti yako!

*Mpendwa*

14 [e]Njoo, mpenzi wangu,
uwe kama swala
au kama ayala kijana
juu ya milima iliyojaa vikolezo.

---

[a]**8:11** Mhu 2:4; Mt 21:33; Isa 7:23
[b]11 Shekeli 1,000 ni kama kilo 11.5.
[c]12 Shekeli 200 ni kama kilo 2.3.
[d]**8:13** Wim 2:14
[e]**8:14** Mit 5:19; Wim 2:8-17

# ISAYA

1 [a]Maono kuhusu Yuda na Yerusalemu ambayo Isaya mwana wa Amozi aliyaona wakati wa utawala wa Uzia, Yothamu, Ahazi na Hezekia, wafalme wa Yuda.

*Taifa Asi*

2 [b]Sikieni, enyi mbingu! Sikilizeni,
enyi dunia!
Kwa maana BWANA amesema:
"Nimewalisha watoto na kuwalea,
lakini wameniasi mimi.
3 [c]Ng'ombe anamjua bwana wake,
naye punda anajua hori la mmiliki
wake,
lakini Israeli hajui,
watu wangu hawaelewi."

4 [d]Lo! Taifa lenye dhambi,
watu waliolemewa na uovu,
uzao wa watenda mabaya,
watoto waliozoelea upotovu!
Wamemwacha BWANA,
Wamemkataa kwa dharau
yeye Aliye Mtakatifu wa Israeli
na kumgeuzia kisogo.

5 [e]Kwa nini mzidi kupigwa?
Kwa nini kudumu katika uasi?
Kichwa chako chote kimejeruhiwa,
moyo wako wote ni mgonjwa.
6 [f]Kutoka wayo wako wa mguu hadi
kwenye utosi wa kichwa
chako
hakuna uzima:
ni majeraha matupu na makovu
na vidonda vitokavyo damu,
havikusafishwa au kufungwa
wala kulainishwa kwa mafuta.

7 [g]Nchi yenu imekuwa ukiwa,
miji yenu imeteketezwa kwa moto;
nchi yenu imeachwa tupu na wageni
mbele ya macho yenu,
imeharibiwa kama vile
imepinduliwa na wageni.
8 [h]Binti Sayuni ameachwa kama
kipenu
katika shamba la mizabibu,
kama kibanda katika shamba la
matikitimaji,
kama mji uliohusuriwa.
9 [i]Kama BWANA Mungu Mwenye
Nguvu Zote[j]
asingelituachia walionusurika,
tungelikuwa kama Sodoma,
tungelifanana na Gomora.

10 [k]Sikieni neno la BWANA,
ninyi watawala wa Sodoma;
sikilizeni sheria ya Mungu wetu,
enyi watu wa Gomora!
11 [l]BWANA anasema, "Wingi wa sadaka
zenu,
ni kitu gani kwangu?

---

[a]**1:1** 1Sam 3:1; Hes 12:6; 2Fal 14:21; 16:1; 1Nya 3:12-13; 2Nya 26:22; 1Sam 22:1, 5; Oba 1:1; Nah 1:1; Isa 40:9; 44:26
[b]**1:2** Hag 1:12; Amu 11:10; Kum 4:26; Yer 42:5; Isa 23:4; 63:16; 65:2; Eze 24:3; Mik 1:2; Isa 63:16; Mal 1:6
[c]**1:3** Yer 4:22; 9:3-6; Hos 2:8; Ay 12:9; Mwa 42:27; Kum 32:28; Isa 42:25; Ay 12:9; Hos 4:1; Isa 48:8; Hos 4:6; 7:9
[d]**1:4** Yer 23:14; Eze 39:7; 2Fal 19:22; Isa 1:2; Za 14:3; Kum 32:15; Isa 5:19; 31:1; 5:18; 9:17; 14:20; Za 119:87
[e]**1:5** Yer 2:20; 30:17; 44:16-17; 2:30; 5:3; Ebr 3:16; Isa 31:6; 44:16-17; Mit 20:30; Mao 2:11
[f]**1:6** Kum 28:35; Yer 8:22; 14:19; 30:17; Mao 2:13; Eze 34:4; Lk 10:34; 2Sam 14:2; Za 45:7; 104:15; 38:3; Isa 61:3; 53:5; 30:26
[g]**1:7** Kum 28:51; Amu 6:3-6; Isa 62:8; 2Fal 18:13; Law 26:34; 26:16; Yer 5:17; Za 109:11
[h]**1:8** Za 9:14; Isa 10:32; 30:17; 49:21; Ay 27:18
[i]**1:9** Rum 9:29; 2Fal 21:14; Mwa 45:7; 19:24; Isa 4:2; 6:13; 27:12; Yer 23:3; Yoe 2:32
[j]9 Bwana Mwenye Nguvu Zote hapa ni Yehova Sabaoth, yaani Bwana wa Majeshi; pia Warumi 9:29 na Yakobo 5:4.
[k]**1:10** Isa 30:9; 28:14; 5:24; 8:20; 13:19; Ufu 11:8; Mwa 13:13; Eze 16:49; Rum 9:29
[l]**1:11** Amo 6:4; Yer 6:20; Ebr 10:4; Za 50:8; 40:6; Ay 22:3; Isa 66:3; 1Sam 15:22; Mal 1:10

Ninazo sadaka za kuteketezwa
nyingi kupita kiasi,
za kondoo dume na mafuta ya
wanyama walionona.
Sipendezwi na damu za mafahali
wala za wana-kondoo na mbuzi.
12 [a]Mnapokuja kujihudhurisha mbele
zangu,
ni nani aliyewataka ninyi mfanye
hivyo,
huku kuzikanyaga nyua zangu?
13 [b]Acheni kuniletea sadaka zisizokuwa
na maana!
Uvumba wenu ni chukizo kwangu.
Miandamo ya Mwezi, Sabato na
makusanyiko ya ibada:
siwezi kuvumilia makusanyiko
yenu maovu.
14 [c]Sikukuu zenu za Miandamo ya
Mwezi, na sikukuu zenu
zilizoamriwa:
moyo wangu unazichukia.
Zimekuwa mzigo kwangu,
nimechoka kuzivumilia.
15 [d]Mnaponyoosha mikono yenu katika
maombi,
nitaficha macho yangu nisiwaone;
hata mkiomba maombi mengi
sitasikiliza.
Mikono yenu imejaa damu;
16 [e]jiosheni na mkajitakase.
Yaondoeni matendo yenu maovu
mbele zangu!
Acheni kutenda mabaya,
17 [f]jifunzeni kutenda mema!
Tafuteni haki,
watieni moyo walioonewa.
Teteeni shauri la yatima,
wateteeni wajane.

18 [g]"Njooni basi tuhojiane,"
asema BWANA.
"Ingawa dhambi zenu ni kama rangi
nyekundu,
zitakuwa nyeupe kama theluji;
ingawa ni nyekundu sana kama
damu,
zitakuwa nyeupe kama sufu.
19 [h]Kama mkikubali na kutii,
mtakula mema ya nchi,
20 [i]lakini kama mkikataa na kuasi,
mtaangamizwa kwa upanga."
Kwa kuwa kinywa cha BWANA
kimenena.

21 [j]Tazama jinsi mji uliokuwa
mwaminifu
umekuwa kahaba!
Mwanzoni ulikuwa umejaa unyofu,
haki ilikuwa inakaa ndani yake,
lakini sasa ni wauaji!
22 [k]Fedha yenu imekuwa takataka,
divai yenu nzuri imechanganywa
na maji.
23 [l]Watawala wenu ni waasi,
rafiki wa wevi,
wote wanapenda rushwa
na kukimbilia hongo.
Hawatetei yatima,
shauri la mjane haliletwi mbele
yao lisikilizwe.

---

[a]**1:12** Kut 23:17; Kum 31:11
[b]**1:13** Mit 15:8; 1Nya 23:31; Hag 2:14; Yer 18:15; 44:8; 1Fal 11:24; Mit 28:9; Yer 7:9; Isa 41:24; 66:3
[c]**1:14** Za 69:3; Kut 12:16; Mal 3:14; Kum 16:1-7; Neh 10:33; Ay 7:12; Hes 28:11-29; Law 23:1-44
[d]**1:15** Ay 27:9; Kum 31:17; 1:45; Mik 3:4; Hos 4:2; Isa 57:17; 59:2; Kut 9:29; Yoe 3:21; 1Sam 8:18
[e]**1:16** Yer 4:14; 25:5; Hes 19:11-16; Isa 52:11; Rut 3:3; Yak 4:8; Mt 27:24
[f]**1:17** Mik 6:8; Sef 2:3; Ay 22:9; Isa 33:5; Kut 22:22; Amo 5:14-15; Za 34:14; 72:1; Isa 11:4
[g]**1:18** 1Sam 2:25; Isa 41:21; 55:7; Ufu 7:14; Za 51:7; Isa 43:9; 41:1; 43:26
[h]**1:19** Ezr 9:12; Za 34:10; Ay 36:11; Isa 50:10; 62:9; Kum 30:15-16; Isa 58:14; 65:13; 30:32
[i]**1:20** Yer 17:27; Hes 23:19; Ay 15:22; 1Sam 12:15; Isa 3:25; 21:17; 34:16; 27:1; 65:12
[j]**1:21** Isa 57:3-9; Yer 2:20; 3:2-9; 13:27; Eze 23:3; Hos 2:1-13; Amo 6:12; Isa 46:13; 59:14; Mit 6:17
[k]**1:22** Za 119:119
[l]**1:23** Kum 19:14; Amo 5:8; Yer 5:28; Mik 2:1-2; 6:12; Kut 23:8; Isa 10:2; Eze 22:6-7; Isa 1:2; Mik 3:9; Amo 5:12; Hab 1:4

24 [a]Kwa hiyo Bwana, BWANA Mwenye Nguvu Zote,
Mwenye Nguvu wa Israeli, asema hivi:
"Lo, nitapata faraja kutoka kwa adui zangu
na kujilipizia kisasi juu ya watesi wangu.
25 [b]Nitauelekeza mkono wangu dhidi yenu,
nitawasafisha takataka zenu zote
na kuwaondolea unajisi wenu wote.
26 [c]Nitawarudishia waamuzi wenu kama ilivyokuwa siku za zamani,
nao washauri wenu kama ilivyokuwa mwanzoni.
Baadaye utaitwa,
Mji wa Haki,
Mji Mwaminifu."
27 [d]Sayuni itakombolewa kwa haki,
wale waliomo ndani yake waliotubu kwa uaminifu.
28 [e]Lakini waasi na wenye dhambi wote wataangamizwa,
nao wanaomwacha BWANA wataangamia.

29 [f]"Mtaaibika kwa sababu ya hiyo mialoni
ambayo mlifurahia,
mtafadhaika kwa sababu ya bustani mlizozichagua.
30 [g]Mtakuwa kama mwaloni wenye majani yanayonyauka,
kama bustani isiyokuwa na maji.
31 [h]Mtu mwenye nguvu atatoweka kama majani makavu yawakayo moto,
na kazi yake kama cheche ya moto;
vyote vitaungua pamoja,
wala hakuna wa kuuzima huo moto."

### *Mlima Wa Bwana*

**(Mika 4:1-3)**

2 [i]Hili ndilo alililoliona Isaya mwana wa Amozi kuhusu Yuda na Yerusalemu:
2 [j]Katika siku za mwisho

mlima wa Hekalu la BWANA utaimarishwa
kama mlima mkuu miongoni mwa milima yote,
utainuliwa juu ya vilima,
na mataifa yote yatamiminika huko.

3 [k]Mataifa mengi yatakuja na kusema,

"Njooni, twendeni mlimani mwa BWANA,
kwenye nyumba ya Mungu wa Yakobo.
Atatufundisha njia zake,
ili tuweze kuenenda katika mapito yake."
Sheria itatoka Sayuni,
neno la BWANA litatoka Yerusalemu.
4 [l]Atahukumu kati ya mataifa
na ataamua migogoro ya mataifa mengi.

[a]**1:24** Mwa 49:24; Isa 34:2, 8; 47:3; 59:17; 63:4; Yer 51:6; Eze 5:13; Kum 32:43
[b]**1:25** Yer 9:7; 6:29; Ufu 3:19; Isa 48:10; Kum 28:63; Za 78:38; 2Nya 29:15; Eze 22:22; Za 119:119
[c]**1:26** Mik 4:8; Zek 8:3; Yer 31:23; 33:7; Kum 9:24; Mwa 32:28; Isa 32:16; 46:13; 4:3; 48:2
[d]**1:27** Isa 31:6; 59:20; 35:10; 41:14; 62:12; 63:4; 30:15; Hos 2:19; Eze 18:30
[e]**1:28** Yer 4:18; 44:12; 2The 1:8-9; Isa 33:14; 43:27; 48:8; 16:2; Kum 32:18; 32:15; Za 9:5; Yer 16:4
[f]**1:29** Eze 6:13; Hos 4:13; Isa 65:3; 42:17; 44:9; 57:5; Za 97:7; Yer 10:14; Za 97:7
[g]**1:30** Za 1:3
[h]**1:31** Isa 4:4; 5:24; 9:18-19; 24:6; 33:14; 66:15-16, 24; Yer 5:14; 7:20; Mal 3:2; Mt 25:41
[i]**2:1** Isa 1:1
[j]**2:2** Dan 2:35; 11:45; Yoe 3:17; Mdo 2:17; Isa 11:9; 65:9; Zek 14:10; Yer 16:19
[k]**2:3** Zek 8:21; Lk 24:47; Yn 4:22; Isa 33:22; 45:23; Yer 3:17; Kum 33:19
[l]**2:4** Hos 2:18; Yer 30:11; Za 96:13; 51:4; 46:9; Yoe 3:10; Mwa 49:10; Zek 9:10

Watafua panga zao ziwe majembe,
na mikuki yao kuwa miundu ya
kukata matawi.
Taifa halitainua upanga dhidi ya
taifa jingine,
wala hawatajifunza vita tena.

5 [a]Njooni, enyi nyumba ya Yakobo,
tutembeeni katika nuru ya
BWANA.

*Siku Ya BWANA*

6 [b]Umewatelekeza watu wako,
nyumba ya Yakobo.
Wamejaa ushirikina utokao
Mashariki,
wanapiga ramli kama Wafilisti
na wanashikana mikono na
wapagani.
7 [c]Nchi yao imejaa fedha na dhahabu,
hakuna mwisho wa hazina zao.
Nchi yao imejaa farasi,
hakuna mwisho wa magari yao.
8 [d]Nchi yao imejaa sanamu,
wanasujudia kazi za mikono yao,
vitu vile vidole vyao
vimevitengeneza.
9 [e]Kwa hiyo mwanadamu atashushwa
na binadamu atanyenyekezwa:
usiwasamehe.

10 [f]Ingieni kwenye miamba,
jificheni ardhini
kutokana na utisho wa BWANA
na utukufu wa enzi yake!

11 [g]Macho ya mtu mwenye majivuno
yatanyenyekezwa
na kiburi cha wanadamu
kitashushwa,
BWANA peke yake ndiye
atakayetukuzwa siku hiyo.

12 [h]BWANA Mwenye Nguvu Zote anayo
siku aliyoiweka akiba
kwa wote wenye kujivuna na
wenye kiburi,
kwa wote wanaojikweza
(nao watanyenyekezwa),
13 [i]kwa mierezi yote ya Lebanoni iliyo
mirefu sana,
na mialoni yote ya Bashani,
14 [j]kwa milima yote mirefu
na vilima vyote vilivyoinuka,
15 [k]kwa kila mnara ulio mrefu sana
na kila ukuta wenye ngome,
16 [l]kwa kila meli ya biashara,[m]
na kila chombo cha baharini cha
fahari.
17 [no]Majivuno ya mwanadamu
yatashushwa,
na kiburi cha wanadamu
kitanyenyekezwa,
BWANA peke yake ndiye atatukuzwa
siku hiyo,
18 [p]nazo sanamu zitatoweka kabisa.

---

[a]**2:5** Isa 60:19-20; 1Yn 1:5-7; Isa 58:1; 60:1
[b]**2:6** Kum 18:10, 14; 31:17; Yer 12:7; 2Nya 16:7; Isa 44:25; 2Fal 16:7; Kum 31:17
[c]**2:7** Mwa 41:43; Kum 17:16; Mik 5:10; Za 17:14; Isa 31:1; Kum 17:17
[d]**2:8** Isa 10:9-11; 17:8; 44:17; Ufu 9:20; 2Nya 32:19; Mik 5:13; Isa 44:17; Za 135:15
[e]**2:9** Za 62:9; Isa 13:11; 5:15; 2:11, 17; Hes 4:5; Neh 4:5
[f]**2:10** Ufu 6:15-16; Nah 3:11; Za 145:12; Isa 2:19; 2The 1:9
[g]**2:11** Isa 24:21-23; 37:23; 10:12; 5:15; Eze 31:10; Oba 1:8; Neh 9:29; Ay 40:11; Za 46:10; Hab 2:5
[h]**2:12** Za 76:12; 59:12; Eze 7:7; Ay 40:11; Isa 13:6-9; 34:8; Yer 30:7; Mao 1:12; 2Sam 22:28; Yoe 1:15; Amo 5:18
[i]**2:13** Amu 9:15; Isa 10:33, 34; 29:17; Eze 27:5; Za 22:12; Zek 11:2
[j]**2:14** Isa 30:25; 40:4
[k]**2:15** Isa 25:2, 12; 30:25; 32:14; 33:18; Sef 1:16
[l]**2:16** Mwa 10:4; 1Fal 10:22; 9:26
[m]16 Au: ya Tarshishi (ona pia 1Fal 10:22; 22:48; 2Nya 9:21; 20:36; Isa 60:9.)
[n]**2:17** 2Sam 22:28; Ay 40:11
[o]**2:17** Nah 3:13; Ebr 10:31; Kum 2:25; Isa 11:10, 15
[p]**2:18** Kum 9:21; Mik 5:13; Eze 36:25; Isa 21:9; Yer 10:11; 1Sam 5:2

[19] [a]Watu watakimbilia kwenye
mapango ndani ya miamba,
na kwenye mahandaki ardhini
kutokana na utisho wa BWANA
na utukufu wa enzi yake,
ainukapo kuitikisa dunia.
[20] [b]Siku ile, watu watawatupia
panya na popo
sanamu zao za fedha na za dhahabu,
walizozitengeneza ili waziabudu.
[21] [c]Watakimbilia kwenye mapango
miambani
na kwenye nyufa za miamba
kutokana na utisho wa BWANA
na utukufu wa enzi yake,
ainukapo kuitikisa dunia.

[22] [d]Acheni kumtumainia mwanadamu,
ambaye hana kitu ila pumzi katika
pua zake.
Yeye ana thamani gani?

*Hukumu Juu Ya Yerusalemu Na Yuda.*

3 [e]Tazama sasa, Bwana,
BWANA Mwenye Nguvu Zote,
yu karibu kuwaondolea Yerusalemu
na Yuda
upatikanaji wa mahitaji na
misaada,
upatikanaji wote wa chakula na
tegemeo lote la maji,
[2] [f]shujaa na mtu wa vita,
mwamuzi na nabii,
mwaguzi na mzee,
[3] [g]jemadari wa kikosi cha watu
hamsini
na mtu mwenye cheo, mshauri,
fundi stadi na mlozi mjanja.

[4] [h]Nitawafanya wavulana wawe
maafisa wao,
watoto ndio watakaowatawala.
[5] [i]Watu wataoneana wao kwa wao:
mtu dhidi ya mtu, na jirani dhidi
ya jirani yake.
Kijana atainuka dhidi ya mzee,
mtu mnyonge dhidi ya mtu
mwenye heshima.

[6] Mtu atamkamata mmoja wa ndugu
zake
katika nyumba ya baba yake na
kusema,
"Unalo joho, sasa uwe kiongozi
wetu,
tawala lundo hili la magofu!"
[7] [j]Lakini siku hiyo atapiga kelele
akisema,
"Sina uponyaji.
Sina chakula wala mavazi katika
nyumba yangu,
msinifanye niwe kiongozi wa
watu."

[8] [k]Yerusalemu inapepesuka,
Yuda inaanguka;
maneno yao na matendo yao ni
kinyume na BWANA,
wakiudharau uwepo wake
uliotukuka.
[9] [l]Nyuso zao zinavyoonekana
zinashuhudia dhidi yao,
hujivunia dhambi yao kama
Sodoma,
wala hawaifichi.

---

[a]**2:19** Hos 10:8; Nah 1:3-6; Ay 9:6; 30:9; Ebr 12:26; Hab 3:6; Amu 6:2; Isa 7:19; 14:16; Ay 30:6; Lk 23:30; Ufu 6:15
[b]**2:20** Law 11:19; Eze 36:25; 7:19-20; 14:6; Ufu 9:20; Isa 2:11; Ay 22:24
[c]**2:21** Kut 33:22; Za 145:12; Isa 33:10; 2:19
[d]**2:22** Mit 23:4; Yer 17:5; Yak 4:14; Ay 12:19; Za 119:8-9; Isa 51:12; 40:15; Za 18:42; 118:6, 8; 146:3
[e]**3:1** Law 26:26; Eze 4:16; Amo 4:6; Yer 37:21; Za 18:18; Isa 5:13; 65:13
[f]**3:2** Eze 17:13; Isa 9:14-15; 2Fal 24:14; Kum 18:10
[g]**3:3** Ay 22:8; 2Fal 24:14; Mhu 10:11; Yer 8:17; 2Fal 1:9
[h]**3:4** Mhu 10:16
[i]**3:5** Za 28:3; Yer 9:8; Isa 9:19; Mik 7:2-6
[j]**3:7** Yer 30:12; Hos 5:13; Isa 2:11; 24:2; Eze 34:4; Yoe 1:16
[k]**3:8** Isa 30:9; 9:15-17; 28:15; 1:7; Ay 1:11; Za 73:9-11; 2Nya 33:6; Isa 65:7
[l]**3:9** Mwa 13:13; 2Nya 34:24; Rum 6:23; Hes 32:23; Isa 59:12; Yer 14:7; Mit 8:36; Hos 5:5

Ole wao!
Wamejiletea maafa juu yao
wenyewe.

10 [a]Waambie wanyofu itakuwa heri
kwao,
kwa kuwa watafurahia tunda la
matendo yao.
11 [b]Ole kwa watu waovu! Maafa yapo
juu yao!
Watalipwa kwa ajili ya yale
mikono yao iliyotenda.

12 [c]Vijana wanawatesa watu wangu,
wanawake wanawatawala.
Enyi watu wangu, viongozi wenu
wanawapotosha,
wanawapoteza njia.

13 [d]BWANA anachukua nafasi yake
mahakamani,
anasimama kuhukumu watu.
14 [e]BWANA anaingia katika hukumu
dhidi ya wazee na viongozi wa
watu wake:
"Ninyi ndio mlioharibu shamba
langu la mizabibu,
mali zilizonyang'anywa maskini
zimo nyumbani mwenu.
15 [f]Mnamaanisha nini kuwaponda watu
wangu
na kuzisaga nyuso za maskini?"
asema Bwana, BWANA Mwenye
Nguvu Zote.

16 [g]BWANA asema,
"Wanawake wa Sayuni wana
kiburi,
wanatembea na shingo ndefu,
wakikonyeza kwa macho yao,
wanatembea kwa hatua za madaha,
wakiwa na mapambo ya njuga
kwenye vifundo vya miguu
yao.
17 [h]Kwa hiyo Bwana ataleta majipu
kwenye vichwa vya
wanawake wa Sayuni;
BWANA atazifanya ngozi za
vichwa vyao kuwa vipara."

18 [i]Katika siku ile Bwana atawanyang'anya
uzuri wao: bangili, tepe za kichwani,
mikufu yenye alama za mwezi mwandamo,
19 [j]vipuli, vikuku, shela, 20 [k]vilemba, mikufu
ya vifundo vya miguu, mshipi, chupa za
manukato na hirizi, 21 [l]pete zenye muhuri,
pete za puani, 22 [m]majoho mazuri, mitandio,
mavazi, kifuko cha kutilia fedha, 23 [n]vioo,
mavazi ya kitani, taji na shali.

24 [o]Badala ya harufu ya manukato
kutakuwa na uvundo;
badala ya mishipi, ni kamba;
badala ya nywele zilizotengenezwa
vizuri, ni upara;
badala ya mavazi mazuri, ni nguo
za magunia;
badala ya uzuri, ni alama ya aibu
kwa chuma cha moto.
25 [p]Wanaume wako watauawa kwa
upanga,
nao mashujaa wako watauawa
vitani.
26 [q]Malango ya Sayuni yataomboleza na
kulia,
ataketi mavumbini akiwa fukara.

---

[a]**3:10** Za 37:17; Yer 22:15; Mwa 15:1; Za 128:2; Kum 12:28; 5:33
[b]**3:11** Kum 28:15-68; Ay 9:13; Isa 57:20; Kum 28:15-68; 2Nya 6:23; Yer 21:14; Mao 5:16; Eze 24:14
[c]**3:12** Yer 25:16; Mik 3:5; Isa 9:16; 19:14; 28:7; Yer 23:13; 25:16
[d]**3:13** Ay 10:2; Za 82:1; Isa 2:4
[e]**3:14** 1Sam 12:7; Yak 2:6; Ay 22:4; 24:9; Isa 25:4; 11:4
[f]**3:15** Za 94:5; Ay 24:14; Isa 10:6; 26:6; 29:19; 32:6; 5:7
[g]**3:16** Wim 3:11; Ay 15:25
[h]**3:17** Eze 27:31; Amo 8:10
[i]**3:18** Mwa 41:42; Amu 8:21; Isa 2:11
[j]**3:19** Mwa 24:47; Eze 16:11-12
[k]**3:20** Kut 39:28; Eze 44:18; 24:17, 23
[l]**3:21** Mwa 24:22; Kut 29:6
[m]**3:22** Rut 3:15
[n]**3:23** Eze 26:10; 23:26; Kut 29:6; Wim 3:11; Isa 61:3; 62:3
[o]**3:24** Es 2:12; Mit 31:24; Law 13:40; Yon 3:5-8; Isa 4:4; 20:2; Ay 1:20; 16:15; Mwa 37:34; Yer 4:8; Mao 2:10
[p]**3:25** Isa 1:20; Yer 15:8
[q]**3:26** Yer 14:2; 4:28; Mao 2:10; Ay 2:13; Isa 14:12, 31; 33:9; 24:4, 7; Za 137:1

4 1 [a]Katika siku ile wanawake saba
watamshika mwanaume
mmoja
wakisema, "Tutakula chakula chetu
wenyewe
na kuvaa nguo zetu wenyewe,
ila wewe uturuhusu tu tuitwe kwa
jina lako.
Utuondolee aibu yetu!"

*Tawi La Bwana*

2 [b]Katika siku ile Tawi la BWANA
litakuwa zuri na lenye utukufu, nalo tunda
la nchi litakuwa fahari na utukufu wa
wale Waisraeli watakaonusurika. 3 [c]Wale
watakaoachwa Sayuni, watakaobaki
Yerusalemu, wataitwa watakatifu, wale
wote ambao wameorodheshwa miongoni
mwa walio hai huko Yerusalemu. 4 [d]Bwana
atausafisha uchafu wa wanawake wa
Sayuni, atatakasa madoa ya damu kutoka
Yerusalemu kwa Roho ya hukumu na Roho
ya moto. 5 [e]Kisha BWANA ataumba juu ya
Mlima wote wa Sayuni, na juu ya wale wote
wanaokusanyika hapo, wingu la moshi
wakati wa mchana, na kung'aa kwa miali
ya moto wakati wa usiku, nako juu ya huo
utukufu wote kutatanda kifuniko cha ulinzi.
6 [f]Utakuwa sitara na kivuli kutokana na joto
la mchana, na kuwa mahali pa kujificha
kutokana na dhoruba na mvua.

*Wimbo Wa Shamba La Mizabibu*

5 [g]Nitaimba wimbo kwa ajili ya
mmoja nimpendaye,
kuhusu shamba lake la mizabibu:
Mpendwa wangu alikuwa na shamba
la mizabibu
kwenye kilima chenye rutuba.
2 [h]Alililima na kuondoa mawe
na akaliotesha mizabibu bora
sana.
Akajenga mnara wa ulinzi ndani
yake,
na kutengeneza shinikizo la
kukamulia divai pia.
Kisha akatazamia kupata mazao ya
zabibu nzuri,
lakini lilizaa matunda mabaya tu.

3 [i]"Basi enyi wakazi wa Yerusalemu
na watu wa Yuda,
hukumuni kati yangu na shamba
langu la mizabibu.
4 [j]Ni nini zaidi ambacho kingeweza
kufanyika kwa shamba langu
la mizabibu
kuliko yale niliyofanya?
Nilipotazamia kupata zabibu nzuri,
kwa nini lilizaa zabibu mbaya tu?
5 [k]Sasa nitawaambia lile
nitakalolitendea
shamba langu la mizabibu:
Nitaondoa uzio wake,
nalo litaharibiwa,
nitabomoa ukuta wake,
nalo litakanyagwa.
6 [l]Nitalifanya nchi ya ukiwa
isiyokaliwa na watu,
halitakatiwa matawi wala
kulimwa,
nayo michongoma na miiba itamea
huko,
nitaamuru mawingu yasinyeshe
mvua juu yake."

---

[a]**4:1** Mwa 30:23; 2The 3:12; Isa 13:12; 32:9; 2:11
[b]**4:2** Zek 6:12; Yer 23:5; Eze 36:8; 17:22; Za 72:16; Isa 11:1-5; 52:13; Yer 33:15-16; Isa 2:11; Yer 23:6; Zek 3:8
[c]**4:3** Mao 1:17; Sef 3:13; Rum 11:5; Za 56:8; Lk 10:20; Isa 1:26; Kut 19:6; Yoe 3:1-7
[d]**4:4** Zek 13:9; Isa 3:24; 28:6; 30:30; Mt 3:11; Ufu 7:15
[e]**4:5** Isa 58:8; Kut 13:21-22; Isa 41:20; 65:18; Ufu 14:1; Isa 35:2; Za 18:11; Ufu 7:15
[f]**4:6** Law 23:34-43; Isa 25:4; 30:2; 57:13; 8:14; Za 27:5; 55:8; Eze 11:16; Isa 14:32
[g]**5:1** Za 80:8-9; Yn 15:1; Isa 27:2
[h]**5:2** Kum 32:6; Kut 15:17; Yer 2:21; Mt 21:19; Mk 11:13; Isa 16:8; 27:3; 1Sam 2:9; Ay 24:11; Mt 21:33; Lk 13:6
[i]**5:3** Mt 21:40
[j]**5:4** 2Nya 36:15; Mt 23:37; Yer 2:5-7; 2:21; Mk 6:3-4; Yer 24:2; 29:17
[k]**5:5** Za 80:12; Lk 21:24; Yer 12:10; Isa 6:12; 27:10; 22:5; 10:6; 2Nya 36:21
[l]**5:6** Hos 2:12; Ebr 6:8; Mwa 6:13; Isa 6:13; 49:17; 2Sam 23:6; Isa 7:23-24; Law 26:32; Eze 28:24; 2Sam 1:21; Amo 4:7

7 [a]Shamba la mzabibu la BWANA
Mwenye Nguvu Zote
ni nyumba ya Israeli,
na watu wa Yuda
ni bustani yake ya kumpendeza.
Alitazamia haki, lakini akaona
umwagaji damu,
alitazamia uadilifu, lakini akasikia
vilio vya taabu.

*Ole Na Hukumu*

8 [b]Ole wenu mnaoongeza nyumba
baada ya nyumba
na kuunganisha mashamba baada
ya mashamba
hadi hakuna nafasi iliyobaki,
nanyi mnaishi peke yenu katika
nchi.

9 [c]BWANA Mwenye Nguvu Zote
amesema nikisikia:
"Hakika nyumba kubwa zitakuwa
ukiwa,
nayo majumba ya fahari yatabaki
bila kukaliwa.
10 [d]Shamba la mizabibu la eka kumi
litatoa bathi[e] moja ya divai,
na homeri[f] ya mbegu zilizopandwa
itatoa efa[g] moja tu ya nafaka."

11 [h]Ole wao wale waamkao asubuhi na
mapema
wakikimbilia kunywa vileo,
wale wakawiao sana mpaka usiku,
mpaka wamewaka kwa mvinyo.
12 [i]Wana vinubi na zeze kwenye
karamu zao,
matari, filimbi na mvinyo,
lakini hawayajali matendo ya
BWANA,
wala hawana heshima kwa ajili ya
kazi ya mikono yake.
13 [j]Kwa hiyo watu wangu watakwenda
uhamishoni
kwa sababu ya kukosa ufahamu,
watu wao wenye vyeo watakufa kwa
njaa
na watu wao wengi watakauka
kwa kiu.
14 [k]Kwa hiyo kaburi[l] limeongeza hamu
yake
na kupanua mdomo wake bila
kikomo,
ndani mwake watashuka wakuu wao
na wingi wa watu,
pamoja na wagomvi wao, na
wafanyao sherehe wote.
15 [m]Hivyo mwanadamu atashushwa,
na binadamu kunyenyekezwa,
macho ya wenye majivuno
yatanyenyekezwa.
16 [n]Lakini BWANA Mwenye Nguvu Zote
atatukuzwa
kwa ajili ya haki yake,
naye Mungu Mtakatifu atajionyesha
mwenyewe
kuwa mtakatifu kwa haki yake.
17 [o]Kondoo watajilisha kwenye malisho
yao wenyewe,
wana-kondoo watajilisha katika
magofu ya matajiri.

18 [p]Ole wao wanaovuta dhambi kwa
kamba za udanganyifu
na uovu kama kwa kamba za
mkokoteni,

---

[a]**5:7** Isa 37:30; Eze 9:9; 22:29; Za 80:8; Isa 17:10; 10:2; 29:21; 61:8; Za 12:5
[b]**5:8** Yer 22:13; Isa 24:16; 6:5; 10:1; Hab 2:9-12; Ay 20:19; Mik 2:2
[c]**5:9** Isa 6:11-12; Mt 23:38; Yer 44:11; Isa 22:14; Mt 23:38
[d]**5:10** Law 27:16; Kum 28:38; Zek 8:10; Law 26:26; 27:16
[e]10 Bathi moja ni sawa na lita 22.
[f]10 Homeri moja ni sawa na lita 220.
[g]10 Efa moja ni sawa na lita 22.
[h]**5:11** 1Sam 25:36; Mit 23:29-30
[i]**5:12** 1Sam 12:24; Ay 34:27; Eze 26:13; Amo 6:5-6; Isa 24:8; Ay 21:12; Za 28:5; 68:25
[j]**5:13** Isa 49:21; 1:3; 3:3; Mit 10:21; Hos 4:6; Rum 1:28; Ay 22:8
[k]**5:14** Mit 30:16; Hes 16:30; Isa 22:13; 23:7; 24:8
[l]14 Kaburi hapa maana yake ni Kuzimu, kwa Kiebrania ni Sheol.
[m]**5:15** Isa 2:9-11; 10:33
[n]**5:16** Isa 61:8; Law 10:3; Eze 36:23; Za 97:6; Isa 33:10; 28:17; 30:18; 29:23
[o]**5:17** Sef 2:6, 14; Isa 32:14; 7:25; 17:2
[p]**5:18** Isa 59:4-8; 5:8; Amo 5:8; Yer 17:5; 23:14; Hos 11:4

19 [a]kwa wale wanaosema, "Mungu na
afanye haraka,
aharakishe kazi yake ili tupate
kuiona.
Huo mpango wa Aliye Mtakatifu wa
Israeli na ukamilike,
tena udhihirike ili tupate kuujua."

20 [b]Ole wao wanaoita ubaya ni wema,
na wema ni ubaya,
wawekao giza badala ya nuru,
na nuru badala ya giza,
wawekao uchungu badala ya utamu,
na utamu badala ya uchungu.

21 [c]Ole wao walio na hekima machoni
pao wenyewe,
na kujiona wenye akili machoni
pao wenyewe.

22 [d]Ole wao walio mashujaa kwa
kunywa mvinyo,
nao walio hodari katika
kuchanganya vileo,
23 [e]wale wanaoachilia wenye hatia kwa
kupokea hongo,
lakini huwanyima haki wasio na
hatia.

24 [f]Kwa hiyo, kama ndimi za moto
zirambavyo nyasi,
na kama vile majani makavu
yazamavyo katika miali ya
moto,
ndivyo mizizi yao itakavyooza
na maua yao
yatakavyopeperushwa kama
mavumbi;
kwa kuwa wameikataa sheria ya
BWANA Mwenye Nguvu Zote
na kulisukumia mbali neno la
Aliye Mtakatifu wa Israeli.
25 [g]Kwa hiyo hasira ya BWANA inawaka
dhidi ya watu wake,
mkono wake umeinuliwa na
anawapiga.
Milima inatetemeka,
maiti ni kama takataka kwenye
barabara.

Hata kwa haya yote, hasira yake
haijageukia mbali,
mkono wake bado umeinuliwa
juu.

26 [h]Yeye anainua bendera kwa ajili ya
mataifa yaliyo mbali,
anapiga filimbi kwa ajili ya wale
walio kwenye miisho ya
dunia.
Tazama wamekuja,
kwa kasi na kwa haraka!
27 [i]Hakuna hata mmoja wao
anayechoka wala kujikwaa,
hakuna hata mmoja anayesinzia
wala kulala,
hakuna mkanda uliolegezwa
kiunoni,
hakuna gidamu ya kiatu
iliyokatika.
28 [j]Mishale yao ni mikali,
pinde zao zote zimevutwa,
kwato za farasi wao ziko kama jiwe
la gumegume,
magurudumu ya magari yao
ya vita ni kama upepo wa
kisulisuli.
29 [k]Ngurumo yao ni kama ile ya simba,
wananguruma kama wana simba,

---

[a]**5:19** 2Pet 3:3-4; Eze 12:22; Yer 17:15; Isa 30:11-12; 29:23; 1:4; 60:22
[b]**5:20** Ay 24:13; Amo 5:7; Mwa 18:25; 1Fal 22:8; Za 94:21; Isa 5:8; Mt 6:22-23; Lk 11:22, 34-35
[c]**5:21** Mit 3:7; Rum 12:16; Isa 47:10; 1Kor 3:18-20
[d]**5:22** 1Sam 25:36; Mit 23:20; Isa 22:13; Mit 31:4; Yer 7:18
[e]**5:23** Kut 23:8; Amo 5:12; Yak 5:6; Eze 22:12; Isa 1:17; 29:21; 59:13-15; Za 94:21
[f]**5:24** 2Fal 19:20; Za 107:11; Ay 18:16; Isa 47:14; Ay 24:24; 40:8; 6:10; Isa 1:31; Nah 1:10; 2Fal 19:30
[g]**5:25** 2Fal 22:13; Yer 6:12; 2Fal 9:37; Dan 9:16; Ay 40:11; Kut 19:18; Isa 26:11; 10:17; Ay 40:11; Yer 6:12
[h]**5:26** Za 20:5; Isa 7:18; Zek 10:8; Kum 28:4-9; Isa 13:5; 18:2
[i]**5:27** Yoe 2:7-8; Eze 23:15; Isa 22:21; 40:29-31; 14:31; Ay 12:18
[j]**5:28** Ay 39:23; Za 45:6; 7:12; Eze 26:11; Ay 1:19; Za 25:5; 2Fal 2:1
[k]**5:29** Isa 42:22; 49:24-25; 2Fal 17:25; Mik 5:8; Yer 51:38; Zek 11:3; Sef 3:3; Isa 10:6

wanakoroma wanapokamata
mawindo yao,
na kuondoka nayo pasipo yeyote
wa kuokoa.
30 [a]Katika siku ile watanguruma juu
yake
kama ngurumo za bahari.
Kama mtu akiitazama nchi,
ataona giza na dhiki;
hata nuru itatiwa giza kwa
mawingu.

*Agizo Kwa Isaya*

6 [b]Katika mwaka ule Mfalme Uzia alikufa,
nilimwona Bwana ameketi katika kiti
cha enzi, kilicho juu na kilichotukuzwa
sana, nalo pindo la joho lake likajaza
Hekalu. 2 [c]Juu yake walikuwepo maserafi,
kila mmoja alikuwa na mabawa sita: Kwa
mabawa mawili walifunika nyuso zao,
kwa mengine mawili walifunika miguu
yao, na kwa mawili walikuwa wakiruka.
3 [d]Nao walikuwa wakiitana kila mmoja na
mwenzake:

"Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu
ni BWANA Mwenye Nguvu Zote;
dunia yote imejaa utukufu wake."

4 [e]Kwa sauti zao, miimo ya milango na
vizingiti vilitikisika, nalo Hekalu likajaa
moshi.
5 [f]Ndipo nikalia, "Ole wangu!
Nimeangamia! Kwa kuwa mimi ni mtu
mwenye midomo michafu, nami ninaishi
katikati ya watu wenye midomo michafu,
nayo macho yangu yamemwona Mfalme,
BWANA Mwenye Nguvu Zote."

6 [g]Ndipo mmoja wa wale maserafi
akaruka kunijia akiwa na kaa la moto
linalowaka mkononi mwake, ambalo
alikuwa amelichukua kwa koleo kutoka
madhabahuni. 7 [h]Akanigusa nalo kinywa
changu na kusema, "Tazama, hili limegusa
midomo yako, uovu wako umeondolewa,
nayo dhambi yako imesamehewa."
8 [i]Kisha nikasikia sauti ya Bwana ikisema,
"Nimtume nani? Ni nani atakayekwenda
kwa ajili yetu?"
Nami nikasema, "Mimi hapa. Nitume
mimi!"
9 [jk]Akasema, "Nenda ukawaambie watu
hawa:

" 'Mtaendelea daima kusikiliza,
lakini kamwe hamtaelewa;
mtaendelea daima kutazama,
lakini kamwe hamtatambua.'
10 [l]Fanya mioyo ya watu hawa kuwa
migumu,
fanya masikio yao yasisikie,
na upofushe macho yao.
Wasije wakaona kwa macho yao,
na wakasikiliza kwa masikio yao,
wakaelewa kwa mioyo yao,
nao wakageuka, nikawaponywa."

11 [m]Ndipo nikasema, "Hadi lini, Ee
Bwana?"
Naye akanijibu:

"Hadi miji iwe imeachwa magofu
na bila wakazi,
hadi nyumba zitakapobaki bila watu,
na mashamba yatakapoharibiwa
na kuangamizwa,

---

[a]**5:30** Yer 4:23-28; Za 93:3; Yoe 2:10; Isa 2:1; 2:11; 50:3; Yer 50:42; Ay 21:30; Lk 21:25; 1Sam 2:9; Za 18:28
[b]**6:1** 2Nya 26:22-23; Hes 12:8; Ufu 4:2; 1:13; 2Fal 15:7; Kut 24:10; Ufu 4:2; Yn 12:41; 1Fal 22:19
[c]**6:2** Eze 1:5; 10:15; 1:11; Ufu 4:8
[d]**6:3** Ufu 4:8; Kut 16:7; 15:11; Hes 14:21; Isa 54:5; 11:9; Za 89:9; 72:19; 89:8; Mal 1:11
[e]**6:4** Kut 19:18; Eze 43:5; 44:4; Ufu 15:8
[f]**6:5** Isa 59:3; Yer 9:3-8; 51:57; Hes 17:12; Kum 5:26; Kut 6:12; 24:10; Isa 24:23; 5:8; Lk 5:8; Yer 5:3; 51:57; Ay 42:5
[g]**6:6** Law 10:1; Eze 10:2
[h]**6:7** Dan 10:16; 12:3; 1Yn 1:7; Isa 45:25; Yer 1:9; Law 26:41
[i]**6:8** Mdo 9:4; Ay 40:9; Yer 26:12-15; Mwa 1:26; 22:1; Kut 3:4
[j]**6:9** Mt 13:15; Lk 8:10; Mt 28:19
[k]**6:9** Amo 7:15; Yer 5:21; Eze 3:11; Mt 13:15; Lk 8:10
[l]**6:10** Kut 4:21; Kum 32:39; 29:4; Eze 12:2; Isa 44:18; Yn 12:40; Mk 4:12; 8:18
[m]**6:11** Yer 4:13; Za 79:5; 79:1; Isa 24:10; Yer 35:17; Za 119:11; Law 26:31, 43

[12][a]hadi BWANA atakapokuwa
amekwisha kumpeleka kila
mmoja mbali sana,
na nchi itakapokuwa imeachwa
kabisa.
[13][b]Hata kama sehemu ya kumi ya watu
watabaki katika nchi,
itaharibiwa tena.
Lakini kama vile mvinje na mwaloni
ibakizavyo visiki inapokatwa,
ndivyo mbegu takatifu
itakavyokuwa kisiki katika nchi."

*Ishara Ya Imanueli*

7 [c]Wakati Ahazi mwana wa Yothamu,
mwana wa Uzia, alipokuwa mfalme wa
Yuda, Mfalme Resini wa Aramu,[d] na Peka
mwana wa Remalia mfalme wa Israeli
walipanda kupigana dhidi ya Yerusalemu,
lakini hawakuweza kuushinda.
[2] [e]Wakati huu nyumba ya Daudi
iliambiwa, "Aramu wameungana na
Efraimu." Kwa hiyo mioyo ya Ahazi na
watu wake ilitikiswa, kama miti ya msituni
inavyotikiswa na upepo.
[3] [f]Ndipo BWANA akamwambia Isaya,
"Toka uende, wewe na mwanao Shear-
Yashubu,[g] mkutane na Ahazi huko
mwisho wa mfereji wa Bwawa la Juu,
kwenye barabara iendayo Shamba la Dobi.
[4] [h]Mwambie, 'Uwe mwangalifu, utulie na
usiogope. Usife moyo kwa ajili ya watu
hawa wawili walio kama visiki vya kuni
vifukavyo moshi, kwa ajili ya hasira kali ya
Resini na Aramu na ya mwana wa Remalia.
[5] [i]Aramu, Efraimu na mwana wa Remalia
wamepanga shauri baya ili wakuangamize,
wakisema, [6] [j]"Tuishambulie Yuda, naam,
tuirarue vipande vipande na kuigawa
miongoni mwetu, na kumtawaza mwana
wa Tabeeli awe mfalme juu yake." [7] [k]Lakini
BWANA Mwenyezi asema hivi:

" 'Jambo hili halitatendeka,
halitatokea,
[8] [l]kwa kuwa kichwa cha Aramu ni
Dameski,
na kichwa cha Dameski ni Resini
peke yake.
Katika muda wa miaka sitini na
mitano,
Efraimu atakuwa ameharibiwa
kiasi kwamba hataweza tena kuwa
taifa.
[9] [m]Kichwa cha Efraimu ni Samaria,
na kichwa cha Samaria
ni mwana wa Remalia peke yake.
Kama hamtasimama thabiti katika
imani yenu,
hamtaimarika kamwe.' "

[10] BWANA akasema na Ahazi tena,
[11] [n]"Mwombe BWANA Mungu wako ishara,
iwe kwenye vina virefu sana, au kwenye
vimo virefu sana."
[12] [o]Lakini Ahazi akasema, "Sitaomba;
sitamjaribu BWANA."
[13] [p]Ndipo Isaya akasema, "Sikia sasa, ewe
nyumba ya Daudi! Je, haitoshi kujaribu
uvumilivu wa wanadamu? Je, mtaujaribu
uvumilivu wa Mungu wangu pia? [14] [q]Kwa
hiyo Bwana mwenyewe atawapa ishara:
Bikira atachukua mimba, naye atamzaa

[a]**6:12** Kum 28:64; Yer 30:17; 4:29; Isa 5:5-9; 60:15; 62:4; 62:4
[b]**6:13** Rum 11:5; Ay 14:7; 14:8; Isa 10:22; Kum 14:2; Law 27:30; Isa 5:6; 1:9
[c]**7:1** 2Fal 16:5; 2Nya 28:5; 2Fal 15:25, 37; 1Nya 3:13; Isa 8:6; 7:5, 9
[d]1 Yaani Shamu.
[e]**7:2** 2Sam 7:11; Amo 9:11; Hos 5:8; Isa 16:5; Yer 21:12; Isa 6:4; 22:22; 9:9; Dan 5:6; Hos 5:3
[f]**7:3** 2Fal 18:17; Isa 36:2; 10:21-22
[g]3 Shear-Yashubu maana yake Mabaki Watarudi.
[h]**7:4** Kum 3:2; 20:3; Mao 3:26; Zek 3:2; Mt 24:6; Isa 54:14; 30:15; 21:4; 8:12; 10:24; 51:13; Mwa 15:1
[i]**7:5** Isa 6:1
[j]**7:6** Isa 24:3; 25:8; 28:10
[k]**7:7** Mdo 4:25; Isa 24:3; 25:8; 28:16; 8:10; 40:8; 46:10; 14:24; Za 2:1
[l]**7:8** Mwa 3:15; 14:15; 2Sam 8:6; 2Fal 17:24; Isa 9:11; 17:1-3; 8:4; 17:1-3
[m]**7:9** 2Nya 20:20; Isa 8:6-8; 30:12-14; 9:9; 9:1, 3; Za 20:8; 2Fal 15:29
[n]**7:11** Kum 13:2; Za 139:8; Kut 7:9
[o]**7:12** Kum 4:34
[p]**7:13** Za 63:1; 118:28; Mwa 30:15; Isa 1:14; 49:4; 61:10
[q]**7:14** Mwa 5:13; 21:22; 24:43; Kut 3:12; Lk 2:12; Mt 1:23; Mwa 3:15; 21:22; Lk 1:31

mwana, na ataitwa Imanueli.[a] 15 [b]Atakula
jibini na asali atakapokuwa ameweza
kukataa mabaya na kuchagua mema.
16 [c]Lakini kabla mtoto hajajua kukataa
mabaya na kuchagua mema, nchi ya
wafalme hao wawili unaowaogopa
itafanywa ukiwa. 17 [d]BWANA ataleta juu
yako, juu ya watu wako, na juu ya nyumba
ya baba yako wakati ambao haujawahi
kuwako tangu Efraimu alipojitenga na
Yuda: yeye atawaleteeni mfalme wa
Ashuru."

18 [e]Katika siku ile BWANA atawapigia
filimbi mainzi kutoka vijito vya mbali vya
Misri, na nyuki kutoka nchi ya Ashuru.
19 [f]Wote watakuja na kukaa kwenye
mabonde yenye miteremko, na kwenye
nyufa za miamba, kwenye vichaka vyote
vyenye miiba, na kwenye mashimo yote
ya maji. 20 [g]Katika siku ile Bwana atatumia
wembe ulioajiriwa kutoka ng'ambo ya Mto,[h]
yaani mfalme wa Ashuru, kunyoa nywele za
kichwa chako na malaika ya miguu yako,
na kuziondoa ndevu zako pia. 21 [i]Katika
siku ile, mtu atahifadhi hai ndama mmoja
na kondoo wawili. 22 [j]Kwa ajili ya wingi
wa maziwa watakayotoa, atapata jibini
ya kula. Wote watakaobakia katika nchi
watakula jibini na asali. 23 [k]Katika siku ile,
kila mahali palipokuwa na mizabibu elfu
moja yenye thamani ya shekeli 1,000[l] za
fedha, patakuwa na michongoma na miiba
tu. 24 [m]Watu watakwenda huko wakiwa
na upinde na mshale, kwa maana nchi
itafunikwa na michongoma na miiba.
25 [n]Kuhusu vilima vyote vilivyokuwa
vikilimwa kwa jembe, hamtakwenda huko
tena kwa ajili ya hofu ya michongoma na
miiba. Patakuwa mahali ambapo ng'ombe
wataachiwa huru, na kondoo kukimbia
kimbia.

*Ashuru, Chombo Cha BWANA*

8 [o]BWANA akaniambia, "Chukua gombo
kubwa, uandike juu yake kwa kalamu
ya kawaida jina: Maher-Shalal-Hash-Bazi.[p]
2 [q]Nami nitawaita kuhani Uria, na Zekaria
mwana wa Yeberekia kama mashahidi
wangu waaminifu."

3 [r]Kisha nikaenda kwa nabii mke, naye
akapata mimba, akazaa mwana. Kisha
BWANA akaniambia, "Mwite huyo mtoto
Maher-Shalal-Hash-Bazi. 4 [s]Kabla mtoto
hajaweza kusema 'Baba yangu' au 'Mama
yangu,' utajiri wa Dameski na nyara za
Samaria zitachukuliwa na mfalme wa
Ashuru."

5 BWANA akasema nami tena:

6 [t]"Kwa sababu watu hawa wamekataa
maji ya Shilo yatiririkayo
taratibu
wakamfurahia Resini na mwana
wa Remalia,
7 [u]kwa hiyo Bwana yu karibu kuleta
dhidi yao
mafuriko makubwa ya Mto:[v]
yaani mfalme wa Ashuru na fahari
yake yote.

[a]14 Imanueli maana yake Mungu yu pamoja nasi.
[b]**7:15** Mwa 18:8; Isa 8:4; Kum 1:39; 13:16
[c]**7:16** Isa 8:4; 17:3; Yer 13:5; 7:15; Kum 13:16; 1:39; Hos 5:9-13
[d]**7:17** 2Nya 28:20; 1Fal 12:16; Neh 9:32; 2Nya 7:18; Isa 17:9; 34:13
[e]**7:18** Isa 5:26; 13:5; 7:25
[f]**7:19** Isa 2:19; 7:25; 17:9; 34:13; 55:13
[g]**7:20** Isa 10:15; 29:16; 8:7; 11:15; 2Fal 18:16; Yer 27:6-7; 2:18; 2Sam 10:4; Kum 28:40
[h]20 Yaani Frati.
[i]**7:21** Isa 2:17; Yer 39:10
[j]**7:22** Mwa 18:8; Isa 14:30
[k]**7:23** Isa 5:6; 8:11; 7:2; Hos 2:12
[l]23 Shekeli 1,000 ni kama kilo 11.5.
[m]**7:24** Isa 5:6
[n]**7:25** Isa 5:17; Hag 1:11
[o]**8:1** Kum 27:8; Ay 19:23; Yer 20:3; 51:60; Isa 30:8; 8:3; Hos 1:4
[p]1 Maher-Shalal-Hash-Bazi maana yake ni Haraka kuteka nyara, Upesi kwenye hizo nyara.
[q]**8:2** 2Fal 16:10; Yos 24:22; Rut 4:9; Yer 10:10-12; 32:10
[r]**8:3** Kut 15:20; Mwa 3:15
[s]**8:4** Isa 7:8, 16; Mwa 14:15; Isa 7:8
[t]**8:6** Neh 3:15; Isa 5:24; 7:1; Yn 9:7
[u]**8:7** Isa 7:20; Dan 11:40; Nah 1:8; 2Nya 28:20; Isa 17:12-13; 30:28; Yos 3:15; Isa 10:16
[v]7 Yaani Frati.

Yatafurika juu ya mifereji yake yote,
yatamwagikia juu ya kingo zake zote,
8 [a]na kufika hadi Yuda, yakizunguka kwa kasi juu yake,
yakipita katikati na yakifika hadi shingoni.
Mabawa yake yaliyokunjuliwa
yatafunika upana wa nchi yako,
Ee Imanueli!"[b]

9 [c]Inueni kilio cha vita, enyi mataifa,
na mkavunjwevunjwe!
Sikilizeni, enyi nyote nchi za mbali.
Jiandaeni kwa vita, nanyi mkavunjwevunjwe!
Jiandaeni kwa vita, nanyi mkavunjwevunjwe!
10 [d]Wekeni mikakati yenu, lakini itashindwa;
fanyeni mipango yenu, lakini haitafanikiwa,
kwa maana Mungu yu pamoja nasi.[e]

*Mwogope Mungu*

11 [f]BWANA alisema nami mkono wake wenye nguvu ukiwa juu yangu, akinionya nisifuate njia za taifa hili. Akasema:

12 [g]"Usiite fitina kila kitu ambacho watu hawa hukiita fitina,
usiogope kile wanachokiogopa,
wala usikihofu.
13 [h]BWANA Mwenye Nguvu Zote ndiye peke yake
ikupasaye kumheshimu kuwa mtakatifu,
ndiye peke yake utakayemwogopa,
ndiye peke yake utakayemhofu,
14 [i]naye atakuwa mahali patakatifu;
lakini kwa nyumba zote mbili za Israeli atakuwa
jiwe lile linalosababisha watu kujikwaa
na mwamba wa kuwaangusha.
Kwa watu wa Yerusalemu,
atakuwa mtego na tanzi.
15 [j]Wengi wao watajikwaa;
wataanguka na kuvunjika,
watategwa na kunaswa."

16 [k]Funga ushuhuda na kutia muhuri sheria
miongoni mwa wanafunzi wangu.
17 [l]Nitamngojea BWANA,
ambaye ameificha nyumba ya Yakobo uso wake.
Nitaliweka tumaini langu kwake.

18 [m]Niko hapa, pamoja na watoto ambao
BWANA amenipa. Sisi ni ishara na mfano
wake katika Israeli, kutoka kwa BWANA
Mwenye Nguvu Zote, anayeishi juu ya
Mlima Sayuni.
19 [n]Wakati watu wanapowaambia ninyi
kutafuta ushauri kwa waaguzi na wenye
kuongea na mizimu, ambao hunong'ona
na kunung'unika, je, watu wasingeuliza
kwa Mungu wao? Kwa nini watake shauri
kwa wafu kwa ajili ya walio hai? 20 [o]Kwa
sheria na kwa ushuhuda! Kama hawatasema
sawasawa na neno hili, hawana mwanga
wa mapambazuko. 21 [p]Watazunguka
katika nchi yote, wakiwa na dhiki na njaa.

[a]**8:8** Isa 7:14; 28:15; 18:6; 46:11; Yer 4:13; 48:40
[b]8 Imanueli maana yake Mungu yu pamoja nasi.
[c]**8:9** Isa 17:12-13; Eze 38:7; 38:3; Zek 14:2-3; Ay 34:24; Yer 46:3; 6:4; Zek 14:2; Yos 6:5
[d]**8:10** Ay 5:12; Isa 7:7, 14; Rum 8:31; Mit 19:21; Mt 1:23
[e]10 Kiebrania ni Imanueli.
[f]**8:11** Eze 3:14; 2:8; 1:3
[g]**8:12** Isa 36:6; 7:2; 20:5; 1Pet 3:14; Mt 10:28
[h]**8:13** Hes 20:12; Isa 29:23; Kut 20:20
[i]**8:14** Rum 9:33; Eze 11:16; Isa 24:17-18; Za 118:22; Yer 6:21; Lk 2:34; Isa 4:6; Lk 20:18; Eze 3:20
[j]**8:15** Lk 20:18; Isa 28:13; 59:10; Rum 9:32; Mt 4:19; Lk 20:18; Isa 59:10
[k]**8:16** Dan 8:26; 12:4; Yer 32:14; Rut 4:7; Isa 29:11-12
[l]**8:17** Kum 31:17; Za 27:14; 22:5; Ebr 2:13
[m]**8:18** Mwa 33:5; Ebr 2:13; Kut 3:12; Lk 2:34; Eze 12:6; 24:24; 4:3; Kum 28:46; Eze 12:11; Za 9:11
[n]**8:19** 1Sam 28:8; Isa 29:4; Hes 27:21; Law 19:31
[o]**8:20** Mik 3:6; Isa 60:2; 1:10; Rut 4:7; Lk 16:29; Isa 9:2; 59:9; 9:2
[p]**8:21** Ay 18:12; Kut 22:28; Ay 30:3; Ufu 16:11

Watakapotaabika kwa njaa, watapatwa na hasira kali, nao, wakiwa wanatazama juu, watamlaani mfalme wao na Mungu wao.
22 [a]Kisha wataangalia duniani na kuona tu dhiki na giza, hofu na huzuni tupu, nao watasukumiwa kwenye giza nene kabisa.

### *Kwa Ajili Yetu Mtoto Amezaliwa*

9 [b]Hata hivyo, hapatakuwepo huzuni tena kwa wale waliokuwa katika dhiki. Wakati uliopita aliidhili nchi ya Zabuloni na nchi ya Naftali, lakini katika siku zijazo ataiheshimu Galilaya ya Mataifa, karibu na njia ya bahari, kando ya Yordani:

2 [c]Watu wanaotembea katika giza
wameona nuru kuu,
wale wanaoishi katika nchi ya uvuli
wa mauti,
nuru imewazukia.
3 [d]Umelikuza taifa,
na kuzidisha furaha yao,
wanafurahia mbele zako,
kama watu wanavyofurahia
wakati wa mavuno,
kama watu wafurahivyo
wagawanyapo nyara.
4 [e]Kama vile siku ya kushindwa kwa
Wamidiani,
umevunja nira iliyowalemea,
ile gongo mabegani mwao na
fimbo yake yeye aliyewaonea.
5 [f]Kila kiatu cha askari kilichotumiwa
vitani,
na kila vazi lililovingirishwa
katika damu
vitawekwa kwa ajili ya kuchomwa,
vitakuwa kuni za kuwasha moto.
6 [g]Kwa maana, kwa ajili yetu mtoto
amezaliwa,
tumepewa mtoto mwanaume,
nao utawala utakuwa mabegani
mwake.
Naye ataitwa
Mshauri wa Ajabu, Mungu
Mwenye Nguvu,
Baba wa Milele, Mfalme wa
Amani.
7 [h]Kuongezeka kwa utawala wake na
amani
hakutakuwa na mwisho.
Atatawala katika kiti cha enzi cha
Daudi
na juu ya ufalme wake,
akiuthibitisha na kuutegemeza
kwa haki na kwa adili,
tangu wakati huo na hata milele.
Wivu wa BWANA Mwenye Nguvu
Zote
utatimiza haya.

### *Hasira Ya BWANA Dhidi Ya Israeli*

8 Bwana ametuma ujumbe dhidi ya
Yakobo,
utamwangukia Israeli.
9 [i]Watu wote watajua hili:
Efraimu na wakazi wa Samaria,
wanaosema kwa kiburi
na majivuno ya mioyo,
10 [j]"Matofali yameanguka chini,
lakini tutajenga tena kwa mawe
yaliyochongwa,
mitini imeangushwa,
lakini tutapanda mierezi badala
yake."
11 [k]Lakini BWANA amemtia nguvu adui
wa Resini dhidi yao
na kuchochea watesi wao.

---

[a]**8:22** Ay 15:24; 3:13; Isa 5:30; Ufu 16:10; Mt 25:30
[b]**9:1** 2Fal 15:29; 1Nya 5:26; Law 26:24; Ay 15:24
[c]**9:2** Mt 4:15-16; Eze 5:8; Mal 4:2; Yn 8:12; Za 82:5; 107:10-14; 36:9; Isa 8:20; Efe 5:8
[d]**9:3** Ay 12:23; Isa 25:9; Kut 15:9; Za 119:162; 4:7; Yos 22:8
[e]**9:4** Amu 7:22-25; Nah 1:13; Isa 10:26-27; Mt 11:30; Isa 60:18; Ay 34:24; Isa 37:36-38; 14:24; Yer 2:20; Za 81:6
[f]**9:5** Isa 2:4
[g]**9:6** Ebr 13:20; Mwa 3:15; Ay 15:8; Amu 13:18; Mt 28:18; Za 24:8; Lk 2:14; Mwa 3:15
[h]**9:7** Dan 2:44; Yn 12:34; Yer 23:5; 2Fal 19:31; Za 85:8; 1Kor 15:25; 2Sam 7:13
[i]**9:9** Isa 7:9; Eze 2:4; Zek 7:11; Isa 2:4
[j]**9:10** Mwa 11:3; Amo 7:14; Lk 19:14; 1Fal 7:2-3
[k]**9:11** Isa 7:8

12 [a]Waashuru kutoka upande wa
mashariki
na Wafilisti kutoka upande wa
magharibi
wameila Israeli kwa kinywa
kilichopanuliwa.

Hata kwa haya yote, hasira yake
haijageukia mbali,
mkono wake bado umeinuliwa
juu.

13 [b]Lakini watu hawajamrudia yeye
aliyewapiga,
wala hawajamtafuta Bwana
Mwenye Nguvu Zote.
14 [c]Kwa hiyo Bwana atakatilia mbali
kutoka Israeli kichwa na
mkia,
tawi la mtende na tete katika siku
moja.
15 [d]Wazee na watu mashuhuri ndio
vichwa,
nao manabii wanaofundisha uongo
ndio mkia.
16 [e]Wale wanaowaongoza watu hawa
wanawapotosha,
nao wale wanaoongozwa
wamepotoka.
17 [f]Kwa hiyo Bwana hatawafurahia
vijana,
wala hatawahurumia yatima na
wajane,
kwa kuwa kila mmoja wao hamchi
Mungu, nao ni waovu,
na kila kinywa kinanena upotovu.

Hata kwa haya yote, hasira yake
haijageukia mbali,
mkono wake bado umeinuliwa
juu.

18 [g]Hakika uovu huwaka kama moto;
huteketeza michongoma na miiba,
huwasha moto vichaka vya msituni,
hujiviringisha kuelekea juu kama
nguzo ya moshi.
19 [h]Kwa hasira ya Bwana Mwenye
Nguvu Zote
nchi itachomwa kwa moto,
nao watu watakuwa kuni za
kuchochea moto.
Hakuna mtu atakayemhurumia
ndugu yake.
20 [i]Upande wa kuume watakuwa
wakitafuna,
lakini bado wataona njaa;
upande wa kushoto watakuwa
wakila,
lakini hawatashiba.
Kila mmoja atajilisha kwa nyama ya
mtoto wake mwenyewe:
21 [j]Manase atamla Efraimu,
naye Efraimu atamla Manase;
nao pamoja watakuwa kinyume na
Yuda.

Hata kwa haya yote, hasira yake
haijageukia mbali,
mkono wake bado umeinuliwa
juu.

10 [k]Ole wao wawekao sheria zisizo
za haki,
kwa wale watoao amri za kuonea,
2 [l]kuwanyima maskini haki zao
na kuzuilia haki za watu wangu
walioonewa,
kuwafanya wajane mawindo yao
na kuwanyang'anya yatima.

---

[a]**9:12** Za 79:7; Isa 5:25; 2Fal 16:6; Ay 40:11
[b]**9:13** Yer 5:3; Amo 4:6-10; Sef 1:16; 2Nya 28:22; Hag 2:17; Dan 9:13; Yer 50:4; Isa 17:7
[c]**9:14** Isa 19:15; Ufu 18:8
[d]**9:15** Isa 3:2-3; 5:13; 28:7; Ay 13:4; Eze 13:2, 22; Mt 24:24
[e]**9:16** Mt 15:14; 23:16, 24; Isa 3:12
[f]**9:17** Amo 8:13; Rum 3:13-14; Yer 13:14; Isa 32:6; Mik 7:2; Isa 5:25; Yer 9:21; 11:22; Isa 27:11; 5:25; Mt 12:34; Yer 48:15; 49:26
[g]**9:18** Za 83:14; Kum 29:23; Isa 1:31; 5:6
[h]**9:19** Mik 7:2-6; Isa 13:9-13; Ay 40:11; Za 97:3; Isa 1:31; Yer 17:27; Isa 3:5
[i]**9:20** Law 26:26; Ay 18:12; Isa 49:26; Zek 11:9
[j]**9:21** Amu 7:22; 12:4; 2Nya 28:6; Isa 5:25
[k]**10:1** Za 58:2; Isa 5:8
[l]**10:2** Isa 3:14; 5:23; Kum 10:18; Ay 6:27; Isa 1:17

3 [a]Mtafanya nini siku ya kutoa hesabu,
wakati maafa yatakapokuja kutoka mbali?
Mtamkimbilia nani awape msaada?
Mtaacha wapi mali zenu?
4 [b]Hakutasalia kitu chochote,
isipokuwa kujikunyata miongoni mwa mateka,
au kuanguka miongoni mwa waliouawa.
Hata kwa haya yote, hasira yake haijageukia mbali,
mkono wake bado umeinuliwa juu.

*Hukumu Ya Mungu Juu Ya Ashuru*

5 [c]"Ole kwa Ashuru, fimbo ya hasira yangu,
ambaye mkononi mwake ana rungu ya ghadhabu yangu!
6 [d]Ninamtuma dhidi ya taifa lisilomjua Mungu,
ninamtuma dhidi ya taifa linalonikasirisha,
kukamata mateka na kunyakua nyara,
pia kuwakanyaga chini kama matope ya barabarani.
7 [e]Lakini hili silo analokusudia,
hili silo alilo nalo akilini;
kusudi lake ni kuangamiza,
kuyakomesha mataifa mengi.
8 [f]Maana asema, 'Je, wafalme wote
si majemadari wangu?
9 [g]Je, Kalno hakutendwa kama Karkemishi?
Hamathi si kama Arpadi,
nayo Samaria si kama Dameski?
10 [h]Kama vile mkono wangu ulivyotwaa falme za sanamu,
falme ambazo vinyago vyao vilizidi vile vya Yerusalemu na Samaria:
11 [i]je, nisiishughulikie Yerusalemu na sanamu zake
kama nilivyoshughulikia Samaria na vinyago vyake?' "

12 [j]Bwana atakapokuwa amemaliza
kazi yake yote dhidi ya Mlima Sayuni na
Yerusalemu, atasema, "Nitamwadhibu
mfalme wa Ashuru kwa ajili ya majivuno
ya ukaidi wa moyo wake na kutazama
kwa macho yenye dharau." 13 [k]Kwa kuwa
anasema:

" 'Kwa nguvu za mkono wangu nimefanya hili,
kwa hekima yangu, kwa sababu nina ufahamu.
Niliondoa mipaka ya mataifa,
niliteka nyara hazina zao,
kama yeye aliye shujaa
niliwatiisha wafalme wao.
14 [l]Kama mtu atiavyo mkono kwenye kiota,
ndivyo mkono wangu ulivyochukua utajiri wa mataifa;
kama watu wakusanyavyo mayai yaliyoachwa,
ndivyo nilivyokusanya nchi zote;
wala hakuna hata mmoja aliyepiga bawa
au kufungua kinywa chake kutoa mlio.' "

15 [m]Je, shoka laweza kujigamba kuwa na nguvu zaidi
kuliko yule anayelitumia,

---

[a]**10:3** Isa 31:3; Hes 9:7; Lk 19:44; Ay 31:14; Za 59:5; Isa 13:6
[b]**10:4** Mao 1:12; Yer 39:6; Isa 24:22; Nah 3:3; Zek 9:11; Isa 5:25; 63:10; Yer 30:24
[c]**10:5** Sef 2:13; Yer 50:23; 51:20; Isa 37:7; Eze 30:24-25; 2Fal 19:21; Isa 7:20; 14:25
[d]**10:6** Isa 9:17-19; 2Nya 28:9; Amu 6:4; Isa 5:29; 2Sam 22:43; Isa 37:26-27; Za 7:5
[e]**10:7** Mwa 50:20; Mdo 4:23-28; Mik 4:12
[f]**10:8** 2Fal 18:24
[g]**10:9** 2Nya 35:20; Mwa 14:15; 2Fal 17:6; Yer 49:24; Hes 13:21; 34:8; Amo 6:2; Mwa 10:10
[h]**10:10** 2Fal 19:18
[i]**10:11** 2Fal 19:13; Isa 36:18-20; 37:10-13
[j]**10:12** 2Fal 19:7, 31; Isa 28:21; 2:8; Yer 50:18; 5:29; Isa 2:11; Eze 28:17; Za 18:27
[k]**10:13** Kut 15:9; Eze 28:4; Dan 4:30; Kum 32:26-27; 8:17; Isa 47:7; 14:13-14
[l]**10:14** Oba 1:4; Hab 2:6-11; Ay 31:25; Yer 49:16; Isa 37:24-25; 2Fal 19:22-24
[m]**10:15** Rum 9:20-21; Isa 7:20; 45:9

au msumeno kujisifu
dhidi ya yule anayeutumia?
Ni kana kwamba fimbo ingeweza
kumwinua yeye aichukuaye,
au mkongojo ungemwinua
mwenye kuutumia!
16 [a]Kwa hiyo Bwana, BWANA Mwenye
Nguvu Zote,
atatuma ugonjwa wa kudhoofisha
kwa askari wake walio hodari,
katika fahari yake moto utawaka
kama mwali wa moto.
17 [b]Nuru ya Israeli itakuwa moto,
Aliye Mtakatifu wao mwali wa
moto;
katika siku moja utaunguza na
kuteketeza miiba
na michongoma yake.
18 [c]Fahari ya misitu yake na mashamba
yenye rutuba
utateketeza kabisa,
kama vile mtu mgonjwa
adhoofikavyo.
19 [d]Nayo miti inayobaki katika misitu
yake itakuwa michache sana
hata mtoto mdogo angeweza
kuihesabu.

*Mabaki Ya Israeli*

20 [e]Katika siku ile, mabaki ya Israeli,
walionusurika wa nyumba ya
Yakobo,
hawatamtegemea tena yeye
aliyewapiga,
lakini watamtegemea kwa kweli
BWANA Aliye Mtakatifu wa Israeli.
21 [f]Mabaki watarudi,[g] mabaki wa
Yakobo
watamrudia Mungu Mwenye
Nguvu.
22 [h]Ingawa watu wako, ee Israeli, ni
wengi kama mchanga wa
pwani,
ni mabaki yao tu watakaorudi.
Maangamizi yamekwisha amriwa,
ni mengi tena ni haki.
23 [i]Bwana, BWANA Mwenye Nguvu
Zote, atatekeleza
maangamizi yaliyoamriwa juu ya
nchi yote.

24 [j]Kwa hiyo, hili ndilo Bwana, BWANA
Mwenye Nguvu Zote asemalo:

"Enyi watu wangu mkaao Sayuni,
msiwaogope Waashuru,
wanaowapiga ninyi kwa fimbo
na kuinua rungu dhidi yenu, kama
Misri ilivyofanya.
25 [k]Bado kitambo kidogo sana hasira
yangu dhidi yenu itakoma,
na ghadhabu yangu itaelekezwa
kwenye maangamizi yao."

26 [l]BWANA Mwenye Nguvu Zote
atawachapa kwa mjeledi,
kama alivyowapiga Wamidiani
katika mwamba wa Orebu,
naye atainua fimbo yake juu ya maji,
kama alivyofanya huko Misri.
27 [m]Katika siku hiyo mzigo wao
utainuliwa kutoka mabegani
mwenu,
na nira yao kutoka shingoni
mwenu;

[a]**10:16** Hes 11:33; Isa 17:14; Za 78:31; Isa 8:7; Yer 21:14
[b]**10:17** Ay 41:21; Isa 37:23; 2Sam 23:6; Isa 9:18; 31:9; Zek 2:5
[c]**10:18** 2Fal 19:23
[d]**10:19** Isa 21:12; 32:19; 17:6; 21:17; 27:13; Yer 44:28
[e]**10:20** Isa 52:6; Zek 9:16; 2Fal 16:7; Eze 7:16; Isa 28:5; 2Nya 14:11; Isa 48:2; Yer 21:2
[f]**10:21** Sef 3:13; Mwa 45:7; Isa 6:13; 9:6
[g]21 Kiebrania ni Shear-Yashubu, pia 22.
[h]**10:22** Rum 9:27-28; Yer 40:2; Dan 9:27; Isa 48:19; Yer 33:22; Isa 11:11
[i]**10:23** Isa 6:12; 28:22; Rum 9:27-28; Dan 9:25
[j]**10:24** Za 87:5-6; Kut 5:14; Isa 7:4; 10:5
[k]**10:25** Isa 17:14; Dan 11:36; Za 30:5; Isa 29:17; Hag 2:6; Isa 24:21; 30:30
[l]**10:26** Isa 37:36-38; Kut 14:16; Isa 30:32; 9:4
[m]**10:27** Isa 9:4; 52:2; Law 26:13; Yer 30:8; Za 66:11; Isa 14:25; 47:6

nira itavunjwa
kwa sababu ya kutiwa mafuta.

28 [a]Wanaingia Ayathi,
wanapita katikati ya Migroni,
wanahifadhi mahitaji huko
Mikmashi.
29 [b]Wanavuka kivukoni, nao
wanasema,
"Tutapiga kambi huko Geba usiku
kucha."
Rama inatetemeka;
Gibea ya Sauli inakimbia.
30 [c]Piga kelele, ee Binti Galimu!
Sikiliza, ee Laisha!
Maskini Anathothi!
31 [d]Madmena inakimbia;
watu wa Gebimu wanajificha.
32 [e]Siku hii ya leo watasimama Nobu;
watatikisa ngumi zao
kwa mlima wa Binti Sayuni,
kwa kilima cha Yerusalemu.

33 [f]Tazama, Bwana, BWANA Mwenye
Nguvu Zote,
atayakata matawi kwa nguvu kuu.
Miti mirefu sana itaangushwa,
ile mirefu itashushwa chini.
34 [g]Atakata vichaka vya msitu kwa
shoka;
Lebanoni itaanguka mbele zake
yeye Mwenye Nguvu.

*Tawi Kutoka Kwa Yese*

11 [h]Chipukizi litatokea kutoka shina
la Yese,
kutoka mizizi yake Tawi litazaa
tunda.
2 [i]Roho wa BWANA atakaa juu yake,
Roho wa hekima na wa ufahamu,
Roho wa shauri na wa uweza,
Roho wa maarifa na wa kumcha
BWANA
3 [j]naye atafurahia kumcha BWANA.

Hatahukumu kwa yale ayaonayo
kwa macho yake,
wala kuamua kwa yale ayasikiayo
kwa masikio yake,
4 [k]bali kwa uadilifu atahukumu
wahitaji,
kwa haki ataamua wanyenyekevu
wa dunia.
Ataipiga dunia kwa fimbo ya kinywa
chake,
kwa pumzi ya midomo yake
atawaua waovu.
5 [l]Haki itakuwa mkanda wake
na uaminifu utakuwa mshipi
kiunoni mwake.

6 [m]Mbwa mwitu ataishi pamoja na
mwana-kondoo,
naye chui atalala pamoja na
mbuzi,
ndama, mwana simba na ng'ombe
wa mwaka mmoja watakaa
pamoja,
naye mtoto mdogo atawaongoza.
7 [n]Ng'ombe na dubu watalisha pamoja,
watoto wao watalala pamoja,
na simba atakula majani makavu
kama maksai.
8 [o]Mtoto mchanga atacheza karibu na
shimo la nyoka,
naye mtoto mdogo ataweka mkono
wake
kwenye kiota cha fira.

---

[a]**10:28** 1Sam 14:2; 13:2; Neh 11:31; Yos 1:11
[b]**10:29** Yos 18:25; 1Sam 13:23; Amu 19:14; Isa 15:5
[c]**10:30** 1Sam 25:44; Neh 11:32; 1Sam 25:44
[d]**10:31** Yos 15:31
[e]**10:32** 1Sam 21:1; Za 9:14; Yer 6:23; Ay 15:25
[f]**10:33** Isa 2:13; 5:15; 18:5; Amo 2:9; Kut 12:2
[g]**10:34** Nah 1:12; Zek 11:2; 2Fal 19:23; Mwa 49:24; Za 93:4; Isa 33:21
[h]**11:1** Zek 6:12; Isa 9:7; Mdo 13:23; Ay 14:7; 2Fal 19:26-30; Isa 27:9; Ufu 5:5
[i]**11:2** Mt 3:16; Yoe 2:28; Yn 16:13; Kut 28:3; Kol 2:3; Amo 3:10; Isa 32:15; 48:16
[j]**11:3** Isa 33:6; Yn 7:24; 2:25
[k]**11:4** Ufu 19:11; Za 72:2-4; Zek 14:12; 2The 2:8; Za 18:8; Isa 14:30; Ufu 19:11; Ay 5:16
[l]**11:5** Isa 25:1; Efe 4:16; Kut 12:11; 1Fal 18:46
[m]**11:6** Hos 2:18; Isa 65:25
[n]**11:7** Ay 40:15
[o]**11:8** Isa 65:20; 14:29; 30:6; 59:5

9 [a]Hawatadhuru wala kuharibu
juu ya mlima wangu mtakatifu
wote,
kwa kuwa dunia itajawa na kumjua
BWANA
kama maji yajazavyo bahari.

10 [b]Katika siku hiyo, Shina la Yese
atasimama kama bendera kwa ajili ya
mataifa. Mataifa yatakusanyika kwake,
na mahali pake pa kupumzikia patakuwa
utukufu. 11 [c]Katika siku hiyo Bwana
atanyoosha mkono wake mara ya pili
kurudisha mabaki ya watu wake waliosalia
kutoka Ashuru, Misri, Pathrosi,[d] Kushi,
Elamu, Babeli, Hamathi na kutoka visiwa
vya baharini.

12 [e]Atainua bendera kwa mataifa
na kuwakusanya Waisraeli
walioko uhamishoni;
atawakusanya watu wa Yuda
waliotawanyika
kutoka pembe nne za dunia.
13 [f]Wivu wa Efraimu utatoweka,
na adui wa Yuda watakatiliwa
mbali;
Efraimu hatamwonea Yuda wivu,
wala Yuda hatakuwa na uadui na
Efraimu.
14 [g]Watawashukia katika miteremko ya
Wafilisti
hadi upande wa magharibi,
kwa pamoja watawateka watu nyara
hadi upande wa mashariki.
Watawapiga Edomu na Moabu,
na Waamoni watatawaliwa nao.
15 [h]BWANA atakausha
ghuba ya bahari ya Misri;
kwa upepo mkavu ataupeleka mkono
wake
juu ya Mto Frati.
Ataugawanya katika vijito saba
ili watu waweze kuuvuka wakiwa
wamevaa viatu.
16 [i]Itakuwepo njia kuu kwa mabaki ya
watu wake
wale waliosalia kutoka Ashuru,
kama ilivyokuwa kwa Israeli
walipopanda kutoka Misri.

*Kushukuru Na Kusifu*

12 [j]Katika siku ile utasema:

“Nitakusifu wewe, Ee
BWANA.
Ingawa ulinikasirikia,
hasira yako imegeukia mbali
nawe umenifariji.
2 [k]Hakika Mungu ni wokovu wangu;
nitamtumaini wala sitaogopa.
BWANA, BWANA, ni nguvu zangu na
wimbo wangu;
amekuwa wokovu wangu.”
3 [l]Kwa furaha mtachota maji
kutoka visima vya wokovu.

4 [m]Katika siku hiyo mtasema:

“Mshukuruni BWANA, mliitie jina
lake;
julisheni miongoni mwa mataifa
yale aliyoyafanya,
tangazeni kuwa jina lake
limetukuka.

[a]**11:9** Hab 2:14; Hes 25:12; Za 98:2-3; Ay 5:23; 1Sam 17:46; Isa 19:21; 52:10
[b]**11:10** Yn 12:32; Rum 15:10-12; Mdo 11:18; Za 116:7; Isa 60:5, 10; 32:17-18; Yer 6:16
[c]**11:11** Mwa 10:22; Zek 10:10; Mik 7:12; Isa 66:19; 10:20; 19:24; Kum 30:4; Hos 11:11
[d]11 Pathrosi ina maana Misri ya Juu.
[e]**11:12** Yn 7:35; Sef 3:10; Eze 28:25; Za 20:5; Isa 14:2; 43:5; Yer 16:15; 31:10
[f]**11:13** 2Nya 28:6; Hos 1:11; Gal 3:28; Yer 3:18; Eze 16:22; 37:16-17, 22
[g]**11:14** Yoe 3:19; Sef 2:8-11; Yer 48:40; 2Nya 26:6; Amu 6:3; 11:14-18; Isa 25:3; Hes 24:18
[h]**11:15** Isa 19:16; 30:32; 7:20; Ufu 16:12; Kut 14:22, 29; Kum 11:10; Yer 50:38; Mwa 41:16
[i]**11:16** Kut 14:26-31; Yer 50:5; Isa 19:23; 35:8; 51:10; 62:10; Mwa 45:7
[j]**12:1** Zek 14:20-21; Isa 25:1; 10:20; Ay 13:16; Za 71:21; 9:1
[k]**12:2** Kut 15:2; Dan 6:23; Za 26:1; 118:14; Isa 17:10; 25:9; 26:4; Ay 13:15
[l]**12:3** Yer 2:13; 17:13; Za 39:6; Yn 4:10, 14; 2Fal 3:17; Kut 15:25
[m]**12:4** Za 80:18; 113:2; Hos 12:5; Kut 3:15; Isa 10:20; 24:15; Yer 10:7

5 [a]Mwimbieni Bwana, kwa kuwa
ametenda mambo makuu,
hili na lijulikane duniani kote.
6 [b]Pazeni sauti mwimbe kwa furaha,
watu wa Sayuni,
kwa maana mkuu ni yeye Aliye
Mtakatifu wa Israeli miongoni
mwenu."

*Unabii Dhidi Ya Babeli*

13 [c]Neno kuhusu Babeli ambalo Isaya mwana wa Amozi aliliona:

2 [d]Twekeni bendera juu ya mlima usio
na kitu,
wapazieni sauti,
wapungieni mkono waingie
katika malango ya wenye
heshima.
3 [e]Nimewaamuru watakatifu wangu;
nimewaita mashujaa wangu
waitimize hasira yangu:
wale wanaoshangilia ushindi
wangu.
4 [f]Sikilizeni kelele juu ya milima,
kama ile ya umati mkubwa wa
watu!
Sikilizeni, makelele katikati ya
falme,
kama mataifa yanayokusanyika
pamoja!
Bwana Mwenye Nguvu Zote
anakusanya
jeshi kwa ajili ya vita.
5 [g]Wanakuja kutoka nchi za mbali
sana,
kutoka miisho ya mbingu,
Bwana na silaha za ghadhabu yake,
kuangamiza nchi yote.

6 [h]Ombolezeni, kwa maana siku ya
Bwana i karibu,
itakuja kama uharibifu kutoka
kwa Mwenyezi.[i]
7 [j]Kwa sababu ya hili, mikono yote
italegea,
moyo wa kila mtu utayeyuka.
8 [k]Hofu itawakamata,
uchungu na maumivu makali
yatawashika,
watagaagaa kama mwanamke aliye
na utungu wa kuzaa.
Watatazamana kwa hofu kila mtu na
mwenzake,
nyuso zao zikiwaka kama moto.

9 [l]Tazameni, siku ya Bwana inakuja,
siku katili, yenye ghadhabu na
hasira kali,
kuifanya nchi kuwa ukiwa
na kuwaangamiza wenye dhambi
waliomo ndani yake.
10 [m]Nyota za mbinguni na makundi ya
nyota
havitatoa mwanga wake.
Jua linalochomoza litatiwa giza
na mwezi hautatoa nuru yake.
11 [n]Nitauadhibu ulimwengu kwa ajili ya
uovu wake,
waovu kwa ajili ya dhambi zao.
Nitakomesha majivuno ya wenye
kiburi,
na nitakishusha kiburi cha watu
wakatili.

---

[a]**12:5** Kut 15:1; Za 98:1
[b]**12:6** Za 78:41; Eze 39:7; Sef 3:14-17; Za 46:5; 98:4; Mwa 21:6; Isa 48:20; Zek 2:10
[c]**13:1** Isa 14:28; 21:9; 48:14; Ufu 14:8; Mwa 10:10; Mal 1:1; Isa 14:4; 46:1-2
[d]**13:2** Za 20:5; 50:2; Yer 51:27; 51:58; 50:2; Isa 24:12; 45:2; 24:2
[e]**13:3** Yer 51:11; Yoe 3:11; Za 149:2; Isa 21:2; Kum 5:28; Ay 40:11
[f]**13:4** Yoe 3:14; Za 46:6; Isa 42:13; 47:4; Yer 50:41
[g]**13:5** Yos 6:17; Isa 5:26; 34:2; 54:16; 10:25; 34:2; Yer 50:25
[h]**13:6** Amo 5:18; Eze 30:2; Yak 5:1; Isa 2:12; 14:31; 10:3; 15:2
[i]6 Mwenyezi hapa ina maana ya Shaddai kwa Kiebrania.
[j]**13:7** Eze 21:7; Yos 2:11; 2Fal 19:26; Ay 4:3; Yer 47:3
[k]**13:8** Nah 2:10; Yoe 2:6; Za 31:13; Isa 21:4; Za 48:5; Kut 15:14; Mwa 3:16; Yn 16:21
[l]**13:9** Isa 2:12; Yer 6:23; 51:2; Isa 9:19; 66:16; Yer 25:31; Yoe 3:2
[m]**13:10** Kut 10:22; Ufu 8:12; Amo 5:20; Zek 14:7; Ay 9:7; Mt 24:29; Isa 5:30; 24:23
[n]**13:11** Isa 3:11; 26:21; 65:6-7; 49:25-26; Za 125:3; Mit 16:18; Dan 5:23; 4:37; Eze 28:2

12 [a]Nitawafanya wanadamu kuwa
adimu kuliko dhahabu safi,
watakuwa wachache sana kuliko
dhahabu ya Ofiri.
13 [b]Kwa hiyo nitazifanya mbingu
zitetemeke,
nayo dunia itatikisika kutoka
mahali pake
katika ghadhabu ya BWANA Mwenye
Nguvu Zote,
katika siku ya hasira yake
iwakayo.

14 [c]Kama swala awindwaye,
kama kondoo wasio na mchungaji,
kila mmoja atarudi kwa watu wake
mwenyewe,
kila mmoja atakimbilia nchi yake
ya kuzaliwa.
15 [d]Yeyote atakayetekwa atapasuliwa
tumbo,
wote watakaokamatwa watauawa
kwa upanga.
16 [e]Watoto wao wachanga watavunjwa
vipande vipande
mbele ya macho yao;
nyumba zao zitatekwa
na wake zao watatendwa jeuri.

17 [f]Tazama, nitawachochea Wamedi
dhidi yao,
ambao hawajali fedha
wala hawafurahii dhahabu.
18 [g]Mishale yao itawaangusha vijana,
hawatakuwa na huruma kwa
watoto wachanga
wala hawataangalia watoto kwa
huruma.
19 [h]Babeli, johari ya falme,
utukufu wa kiburi cha Wababeli,[i]
itaangushwa na Mungu
kama Sodoma na Gomora.
20 [j]Hautakaliwa na watu kamwe
wala watu hawataishi humo kwa
vizazi vyote.
Hakuna Mwarabu atakayepiga hema
lake huko,
hakuna mchungaji
atakayepumzisha makundi
yake huko.
21 [k]Lakini viumbe wa jangwani
watalala huko,
mbweha watajaza nyumba zake,
bundi wataishi humo
nao mbuzi-mwitu watarukaruka
humo.
22 [l]Fisi watalia ndani ya ngome zake,
mbweha ndani ya majumba yake
ya kifahari.
Wakati wake umewadia,
na siku zake hazitaongezwa.

### *Yuda Kufanywa Upya*

14 [m]BWANA atamhurumia Yakobo,
atamchagua Israeli
tena,
na kuwakalisha katika nchi yao
wenyewe.
Wageni wataungana nao
na kujiunga na nyumba ya
Yakobo.
2 [n]Mataifa watawachukua
na kuwaleta mahali pao wenyewe.

---

[a]**13:12** Isa 4:1; Mwa 10:29
[b]**13:13** Hag 2:6; Za 102:26; Isa 9:19; 14:16; 34:4; Mt 24:7; Ay 9:5; 9:6; Mk 13:8
[c]**13:14** Nah 3:7; Yn 10:11; Yer 51:9; 46:16; 4:9; Mit 6:5; Isa 17:13; 21:15; 33:3; Mt 9:36
[d]**13:15** Yer 50:25; 51:4; Isa 14:19
[e]**13:16** Nah 3:10; Hes 16:27; 13:16; Mwa 34:29; 2Fal 8:12
[f]**13:17** 2Fal 18:14-16; Mit 19:24-25; Yer 51:11; 50:9, 41
[g]**13:18** Za 7:12; Isa 41:2; Yer 49:26
[h]**13:19** Dan 4:30; Za 137:8; Ufu 14:8; Mwa 19:24-25; Rum 9:29; Isa 47:5; Dan 2:37-38
[i]19 Wababeli hapa maana yake ni Wakaldayo.
[j]**13:20** Isa 14:23; 34:10-15; 2Nya 17:11; Yer 51:29, 37-43, 62
[k]**13:21** Za 74:14; Ufu 18:2; Yer 14:6; Law 11:16-18; Kum 14:15-17; 2Nya 11:15
[l]**13:22** Isa 34:14; Kum 32:25; Yer 48:16; 9:11; Isa 25:2; 32:14; Yer 50:39; Mal 1:3
[m]**14:1** Isa 54:7-8; Zek 10:6; Mwa 18:19; Eze 47:22; Efe 2:12-19; Kut 12:43; Eze 47:22; Zek 8:22-23; Isa 11:10; Yer 3:18; Zek 2:12
[n]**14:2** Isa 11:12; 26:15; 49:7; 49:23; 54:3; 60:9; Sef 3:19; Zek 2:9; Za 49:14

Nayo nyumba ya Israeli itamiliki mataifa
kama watumishi na wajakazi katika nchi ya BWANA.
Watawafanya watekaji wao kuwa mateka,
na kutawala juu ya wale waliowaonea.

3 [a]Katika siku BWANA atakapokuondolea
mateso, udhia na utumwa wa kikatili,
4 [b]utaichukua dhihaka hii dhidi ya mfalme
wa Babeli:

Tazama jinsi mtesi alivyofikia mwisho!
Tazama jinsi ghadhabu yake kali ilivyokoma!
5 [c]BWANA amevunja fimbo ya mwovu,
fimbo ya utawala ya watawala,
6 [d]ambayo kwa hasira waliyapiga mataifa
kwa mapigo yasiyo na kikomo,
nao kwa ghadhabu kali waliwatiisha mataifa
kwa jeuri pasipo huruma.
7 [e]Nchi zote ziko kwenye mapumziko na kwenye amani,
wanabubujika kwa kuimba.
8 [f]Hata misunobari na mierezi ya Lebanoni
inashangilia mbele yako na kusema,
"Basi kwa sababu umeangushwa chini,
hakuna mkata miti atakayekuja kutukata."

9 [g]Kuzimu kote kumetaharuki
kukulaki unapokuja,
kunaamsha roho za waliokufa ili kukupokea,
wote waliokuwa viongozi katika ulimwengu,
kunawafanya wainuke kwenye viti vyao vya kifalme:
wale wote waliokuwa wafalme juu ya mataifa.
10 [h]Wote wataitikia,
watakuambia,
"Wewe pia umekuwa dhaifu, kama sisi tulivyo;
wewe umekuwa kama sisi."
11 [i]Majivuno yako yote yameshushwa mpaka kuzimu,
pamoja na kelele ya vinubi vyako,
mafunza yametanda chini yako,
na minyoo imekufunika.

12 [j]Tazama jinsi ulivyoanguka kutoka mbinguni,
ewe nyota ya asubuhi, mwana wa mapambazuko!
Umetupwa chini duniani,
wewe uliyepata kuangusha mataifa!
13 [k]Ulisema moyoni mwako,
"Nitapanda juu hadi mbinguni,
nitakiinua kiti changu cha enzi
juu ya nyota za Mungu,
nitaketi nimetawazwa
juu ya mlima wa kusanyiko,
kwenye vimo vya juu sana vya Mlima Mtakatifu.
14 [l]Nitapaa juu kupita mawingu,
nitajifanya kama Yeye Aliye Juu Sana."
15 [m]Lakini umeshushwa chini hadi kuzimu,
hadi kwenye vina vya shimo.

---

[a]**14:3** Isa 11:10-12; Ay 3:17; Kut 1:14
[b]**14:4** Hab 2:6; Mik 2:4; Isa 13:19; 9:4
[c]**14:5** Isa 10:15; Za 125:3; 110:2
[d]**14:6** 2Fal 15:29; Isa 10:14; Za 47:3; Isa 47:6
[e]**14:7** Za 126:1-3; Hes 6:26; Yer 50:34; Zek 1:11
[f]**14:8** 1Nya 16:33; Za 65:13; Eze 31:16; 2Fal 19:23; Isa 37:24
[g]**14:9** Mit 30:16; Eze 32:21; Ay 26:5; Zek 10:3; Ay 3:14
[h]**14:10** Eze 26:20; 32:21
[i]**14:11** Ay 7:5; 24:20; Hes 16:30; Mit 30:16; Isa 5:12; Eze 26:13; Amo 6:5; Ay 21:26
[j]**14:12** Isa 34:4; 2Pet 1:19; Ufu 2:28; Lk 10:18; Eze 26:17; Ufu 2:28
[k]**14:13** Mt 11:23; Eze 28:2; 2The 2:4; Dan 8:10; 5:23; Isa 37:24
[l]**14:14** Hes 24:16; 2The 2:4; Ay 20:6; Isa 47:8; Yer 50:29; Dan 11:38; Isa 10:13
[m]**14:15** Mt 11:23; Lk 10:15; Mdo 12:23; Isa 13:6; 47:11; Ay 21:13; Eze 31:16

16 [a]Wale wanaokuona wanakukazia
macho,
wanatafakari hatima yako:
"Je, huyu ndiye yule aliyetikisa
dunia
na kufanya falme zitetemeke,
17 [b]yule aliyeifanya dunia kuwa
jangwa,
aliyeipindua miji yake,
na ambaye hakuwaachia mateka
wake
waende nyumbani?"

18 [c]Wafalme wote wa mataifa wamelala
kwa heshima
kila mmoja katika kaburi lake.
19 [d]Lakini wewe umetupwa nje ya
kaburi lako
kama tawi lililokataliwa,
umefunikwa na waliouawa
pamoja na wale waliochomwa
kwa upanga,
wale washukao mpaka
kwenye mawe ya shimo.
Kama mzoga uliokanyagwa chini ya
nyayo,
20 [e]Hutajumuika nao kwenye
mazishi,
kwa kuwa umeharibu nchi yako
na kuwaua watu wako.

Mzao wa mwovu
hatatajwa tena kamwe.
21 [f]Andaa mahali pa kuwachinjia
wanawe
kwa ajili ya dhambi za baba zao,
wasije wakainuka ili kuirithi nchi
na kuijaza dunia kwa miji yao.

22 [g]BWANA Mwenye Nguvu Zote asema,
"Nitainuka dhidi yao,
nitalikatilia mbali jina lake kutoka
Babeli pamoja na watu wake
walionusurika,
watoto wake na wazao wake,"
asema BWANA.
23 [h]"Nitaifanya kuwa mahali pa bundi,
na kuwa nchi ya matope;
nitaifagia kwa ufagio wa
maangamizi,"
asema BWANA Mwenye Nguvu
Zote.

*Unabii Dhidi Ya Ashuru*

24 [i]BWANA Mwenye Nguvu Zote ameapa,

"Hakika, kama vile nilivyopanga,
ndivyo itakavyokuwa,
nami kama nilivyokusudia, ndivyo
itakavyosimama.
25 [j]Nitamponda Mwashuru katika nchi
yangu,
juu ya milima yangu
nitawakanyagia chini.
Nira yake itaondolewa kutoka kwa
watu wangu,
nao mzigo wake utaondolewa
kutoka mabegani mwao."

26 [k]Huu ndio mpango uliokusudiwa
kwa ajili ya ulimwengu wote,
huu ni mkono ulionyooshwa juu
ya mataifa yote.
27 [l]Kwa kuwa BWANA Mwenye Nguvu
Zote amekusudia,
ni nani awezaye kumzuia?
Mkono wake umenyooshwa,
ni nani awezaye kuurudisha?

---

[a]**14:16** Yer 50:23; Ufu 18:18; Isa 2:19; 13:13; Yoe 3:16
[b]**14:17** Isa 15:6; Za 52:7; 2Fal 15:29; Kut 7:14; Yer 50:33; Ufu 18:18
[c]**14:18** Ay 21:32
[d]**14:19** Isa 22:16-18; Yer 36:30; Isa 34:3; 13:15; Yer 8:1; 41:7-9
[e]**14:20** Ay 18:19; Kum 32:16; Za 21:10; 1Fal 21:19
[f]**14:21** Mwa 9:25; Kut 20:5; Hes 16:27; Law 26:39
[g]**14:22** 2Sam 18:18; 1Fal 14:10; Za 94:16; Ay 18:17-19; Isa 13:18; Za 109:13
[h]**14:23** Law 11:16-18; Sef 2:14; Isa 34:11-15; Yer 25:12; 50:3; 51:62
[i]**14:24** Isa 62:8; Eze 12:25; Mdo 4:28; Isa 45:23; 23:8-9; Dan 4:35; Isa 46:10-11
[j]**14:25** Isa 37:36-37; 10:27; 9:4
[k]**14:26** Kut 15:12; Ay 30:21; Isa 23:9
[l]**14:27** 2Nya 20:6; Ay 40:8; Dan 4:35; Yer 49:20; Kut 14:21

*Unabii Dhidi Ya Wafilisti*

28 Neno hili lilikuja mwaka ule Mfalme Ahazi alipofariki:

29 [a]Msifurahi, enyi Wafilisti wote,
kwamba fimbo iliyowapiga imevunjika;
kutoka mzizi wa huyo nyoka
atachipuka nyoka mwenye sumu kali,
uzao wake utakuwa joka lirukalo,
lenye sumu kali.
30 [b]Maskini kuliko maskini wote watapata malisho,
nao wahitaji watalala salama.
Lakini mzizi wako nitauangamiza kwa njaa,
nayo njaa itawaua walionusurika.

31 [c]Piga yowe, ee lango! Bweka, ee mji!
Yeyukeni, enyi Wafilisti wote!
Wingu la moshi linakuja toka kaskazini,
wala hakuna atakayechelewa katika safu zake.
32 [d]Ni jibu gani litakalotolewa
kwa wajumbe wa taifa hilo?
"BWANA ameifanya imara Sayuni,
nako ndani yake watu wake walioonewa watapata kimbilio."

*Unabii Dhidi Ya Moabu*

15 [e]Neno kuhusu Moabu:

Ari iliyo Moabu imeangamizwa:
imeharibiwa kwa usiku mmoja!
Kiri iliyo Moabu imeangamizwa,
imeharibiwa kwa usiku mmoja!
2 [f]Diboni anakwea hadi kwenye hekalu lake,
mpaka mahali pake pa juu ili walie,
Moabu anaombolezea Nebo na Medeba.
Kila kichwa kimenyolewa
na kila ndevu limeondolewa.
3 [g]Wamevaa nguo za magunia barabarani,
juu ya mapaa na kwenye viwanja
wote wanaomboleza,
wamelala kifudifudi kwa kulia.
4 [h]Heshboni na Eleale wanalia,
sauti zao zinasikika hadi Yahazi.
Kwa hiyo watu wenye silaha wa Moabu wanapiga kelele,
nayo mioyo yao imezimia.

5 [i]Moyo wangu unamlilia Moabu;
wakimbizi wake wanakimbilia Soari,
hadi Eglath-Shelishiya.
Wanapanda njia ya kwenda Luhithi,
wanakwenda huku wanalia;
barabarani iendayo Horonaimu
wanaombolezea maangamizi yao.
6 [j]Maji ya Nimrimu yamekauka
na majani yamenyauka;
mimea imekauka wala hakuna
kitu chochote kibichi kilichobaki.
7 [k]Kwa hiyo mali waliyoipata na kujiwekea akiba
wamezichukua na kuvuka Bonde la Mierebi.
8 [l]Mwangwi wa kilio chao umefika hadi mpakani mwa Moabu,
kilio chao cha huzuni kimefika hadi Eglaimu,
maombolezo yao hadi Beer-Elimu.

---

[a]**14:29** Yos 13:3; Isa 11:8; Kum 8:15; 2Nya 26:6
[b]**14:30** Isa 3:15; 25:4; 7:21-22; 8:21; 9:20; Sef 2:5
[c]**14:31** Isa 3:26; Yer 47:2; Eze 32:30; Isa 13:6; 41:25; Mwa 10:14; Yer 13:20; 46:20-24
[d]**14:32** Za 51:18; Isa 37:9; Yak 2:5; Za 87:2; Isa 28:16; 44:28; 4:6
[e]**15:1** Hes 21:28; 22:3-6; Kum 23:6; Hes 17:12; Yer 51:58; 48:24; 2Fal 3:25
[f]**15:2** Yer 48:35; Law 21:5; Ay 1:20; Hes 21:20; Isa 16:12; 2Sam 10:4; Law 13:40
[g]**15:3** Mao 2:11; Mik 1:8; Isa 3:24; Yos 2:8; Yer 48:38; Isa 14:31; Eze 7:18; Yer 47:2
[h]**15:4** Hes 32:3; 21:23-25; Yos 13:26
[i]**15:5** Isa 16:11; Yer 48:31; 48:3-5; 4:20; Mwa 13:10; Hes 21:29
[j]**15:6** Isa 19:5-7; Za 37:2; Hos 4:3; Yer 48:34; Isa 16:8; 33:9; 14:17; Yer 14:5
[k]**15:7** Isa 30:6; Yer 48:36
[l]**15:8** Hes 21:16

9 [a]Maji ya Dimoni yamejaa damu,
lakini bado nitaleta pigo jingine
juu ya Dimoni:
simba juu ya wakimbizi wa Moabu
na juu ya wale wanaobaki katika
nchi.

*Hali Ya Kukata Tamaa Ya Moabu*

16 [b]Pelekeni wana-kondoo kama
ushuru
kwa mtawala wa nchi,
Kutoka Sela, kupitia jangwani,
hadi mlima wa Binti Sayuni.
2 [c]Kama ndege wanaopapatika
waliofukuzwa kutoka kwenye
kiota,
ndivyo walivyo wanawake wa
Moabu
kwenye vivuko vya Arnoni.

3 [d]"Tupeni shauri,
toeni uamuzi.
Wakati wa adhuhuri,
fanyeni kivuli chenu kama usiku.
Wafficheni watoro,
msisaliti wakimbizi.
4 [e]Waacheni watoro wa Moabu wakae
pamoja nanyi;
kuweni mahali pao pa salama ili
kuepuka mharabu."

Mtesi atafikia mwisho na
maangamizi yatakoma,
aletaye vita atatoweka kutoka
nchi.
5 [f]Kwa upendo kiti cha enzi
kitaimarishwa,
kwa uaminifu mtu ataketi juu
yake,
yeye atokaye nyumba ya Daudi:
yeye ambaye katika kuhukumu
hutafuta haki,
na huhimiza njia ya haki.

6 [g]Tumesikia juu ya kiburi cha Moabu:
kiburi chake cha kujivuna na
udanganyifu,
kiburi chake na ufidhuli wake,
lakini majivuno yake si kitu.
7 [h]Kwa hiyo Wamoabu wanaomboleza,
wanaiombolezea Moabu kwa
pamoja.
Wanaomboleza na kuhuzunika
kwa ajili ya watu wa
Kir-Haresethi.
8 [i]Mashamba ya Heshboni
yananyauka,
pia na mizabibu ya Sibma.
Watawala wa mataifa
wamekanyaga mizabibu iliyo
mizuri sana,
ambayo ilipata kufika Yazeri
na kuenea kuelekea jangwani.
Machipukizi yake yalienea
yakafika hadi baharini.
9 [j]Hivyo ninalia kama Yazeri aliavyo,
kwa ajili ya mizabibu ya Sibma.
Ee Heshboni, ee Eleale,
ninakulowesha kwa machozi!
Kelele za furaha kwa ajili ya tunda
lako lililoiva
na kwa ajili ya mavuno
zimekomeshwa.
10 [k]Furaha na shangwe zimeondolewa
kutoka mashamba ya matunda;
hakuna yeyote aimbaye wala
apazaye sauti
katika mashamba ya mizabibu;
hakuna yeyote akanyagaye zabibu
shinikizoni,
kwa kuwa nimekomesha makelele.

[a]**15:9** 2Fal 17:25; Eze 25:8-11
[b]**16:1** Isa 10:32; Amu 1:36; 2Fal 14:7; 2Nya 32:23; 2Fal 3:4; Oba 1:3
[c]**16:2** Mit 27:8; Hes 21:13-14; Yer 48:40; Hes 21:29
[d]**16:3** 1Fal 18:4
[e]**16:4** Isa 55:7; 9:4; 2:2-4
[f]**16:5** 1Sam 13:14; Mik 4:7; Isa 7:2; Dan 7:14; Mit 20:28; Isa 9:7; Lk 1:32
[g]**16:6** Eze 25:8; Yer 25:21; Law 26:19; Ay 20:6; Sef 2:8; Yer 49:16; Amo 2:1
[h]**16:7** 1Nya 16:3; 2Fal 3:25; Yer 48:20; 49:3; Isa 13:6
[i]**16:8** Ay 8:16; Hes 21:32; 21:25; Isa 15:6; 5:2; Ay 8:16; Za 80:11
[j]**16:9** Isa 15:3; Eze 27:31; Yer 40:12; Ay 7:3; Hes 32:3; Ezr 3:13
[k]**16:10** Isa 24:7-8; Amu 9:27; Ay 24:11; Yer 25:30; Isa 5:2

11 [a]Moyo wangu unaomboleza kwa ajili
ya Moabu kama kinubi,
nafsi yangu yote kwa ajili ya
Kir-Haresethi.
12 [b]Wakati Moabu anapojitokeza mahali
pake pa juu,
anajichosha mwenyewe tu;
anapokwenda mahali pake pa
kuabudia miungu ili kuomba,
haitamfaidi lolote.

13 Hili ndilo neno ambalo BWANA
ameshasema kuhusu Moabu. 14 [c]Lakini
sasa BWANA anasema: "Katika miaka mitatu, kama vile mtumishi aliyefungwa na mkataba angeihesabu, fahari ya Moabu na watu wake wengi watadharauliwa, nao walionusurika watakuwa wachache sana, tena wanyonge."

*Neno Dhidi Ya Dameski*

17 [d]Neno kuhusu Dameski:

"Tazama, Dameski
haitakuwa tena mji
bali itakuwa lundo la magofu.
2 [e]Miji ya Aroeri itaachwa
na itaachiwa mifugo ambayo
italala huko,
bila yeyote wa kuyaogopesha.
3 [f]Mji wenye ngome utatoweka kutoka
Efraimu,
nao uweza wa ufalme kutoka
Dameski;
mabaki ya Aramu yatakuwa
kama utukufu wa Waisraeli,"
asema BWANA Mwenye Nguvu Zote.

4 [g]"Katika siku ile utukufu wa Yakobo
utafifia,
unono wa mwili wake
utadhoofika.
5 [h][i]Itakuwa kama mvunaji
akusanyavyo nafaka
na kuvuna nafaka kwa mikono
yake,
kama wakati mtu aokotapo masazo
ya masuke
katika Bonde la Warefai.
6 [j]Hata hivyo baadhi ya masazo
yatabaki,
kama vile mti wa mzeituni
unavyopigwa,
kukiachwa zeituni mbili au tatu juu
ya matawi kileleni,
nne au tano katika matawi
yazaayo sana,"
asema BWANA, Mungu wa Israeli.

7 [k]Katika siku ile watu watamwangalia
Muumba wao,
na kuelekeza macho yao kwa yule
Aliye Mtakatifu wa Israeli.
8 [l]Hawataziangalia tena madhabahu,
kazi za mikono yao,
nao hawataheshimu nguzo za
Ashera,[m]
na madhabahu za kufukizia
uvumba zilizofanywa kwa
mikono yao.

9 [n]Katika siku ile miji yao iliyo imara,
ambayo waliihama kwa sababu ya Waisraeli,
itakuwa kama mahali palipoachwa pa
vichaka na magugu. Nayo yote itakuwa
ukiwa.

---

[a]**16:11** Isa 15:5; Hos 11:8; Flp 2:1; Ay 30:31; Isa 63:15
[b]**16:12** Za 115:4-7; 1Kor 8:4; Hes 22:4; Isa 15:2; 1Fal 11:7; 18:29
[c]**16:14** Isa 25:10; Yer 48:42; Kum 15:18; 13:16; Isa 20:3; 37:30; Law 19:13
[d]**17:1** Yer 49:23; Mdo 9:2; Kum 13:16; Zek 9:1; Mwa 14:15; Isa 25:2
[e]**17:2** Yer 7:33; Mik 4:4; Isa 5:17; 2Fal 10:33; Isa 7:21; 27:10; Eze 25:5; Law 26:6
[f]**17:3** Isa 7:8, 16; 21:16; Hos 9:11; Isa 8:4; Hos 10:14; Isa 25:2, 12
[g]**17:4** Isa 2:11; 10:16
[h]**17:5** Yoe 3:13; Mt 13:30; Ufu 14:15-19; Isa 33:4; Yer 51:33; Ay 24:24; Yos 17:15
[i]**17:5** Yos 17:15; 1Nya 11:15
[j]**17:6** Kum 4:24; Isa 10:19; 27:12; 24:3
[k]**17:7** Isa 9:13; 12:6; Zek 12:10; Mik 7:7; Isa 2:12; 10:20; Za 95:6
[l]**17:8** 2Nya 32:19; Ufu 9:20; 2Fal 17:10
[m]8 Ashera hapa maana yake ni mungu mke aliyekuwa akiabudiwa pamoja na Baali.
[n]**17:9** Isa 7:19

10 [a]Mmemsahau Mungu Mwokozi
wenu,
hamkumkumbuka Mwamba aliye
ngome yenu.
Kwa hiyo, hata ingawa mlipandikiza
mimea iliyo mizuri sana
na kuotesha mizabibu ya kigeni,
11 [b]hata kama siku ile unapoipandikiza,
unaifanya iote
na asubuhi ile ile unayoipanda,
unaifanya ichipue,
hata hivyo mavuno yatakuwa kama
si kitu
katika siku ile ya ugonjwa na
maumivu yasiyoponyeka.

12 [c]Lo! Ghadhabu ya mataifa mengi,
wanaghadhibika kama bahari
iliyochafuka!
Lo! Makelele ya mataifa
wanavuma kama ngurumo za maji
mengi!
13 [d]Ingawa mataifa yanavuma kama
ngurumo za maji yanayofanya
mawimbi,
wakati anapoyakemea yanakimbia
mbali,
yanafukuzwa mbele ya upepo kama
makapi juu ya milima,
kama jani livingirishwapo na
dhoruba.
14 [e]Wakati wa jioni, hofu ya ghafula!
Kabla ya asubuhi, wametoweka!
Hili ndilo fungu la wale
wanaotupora,
fungu la wale wanaotunyang'anya
mali zetu.

*Unabii Dhidi Ya Kushi*

18 [f]Ole kwa nchi ya mvumo wa
mabawa,[g]
kando ya mito ya Kushi,
2 [h]iwapelekayo wajumbe wake kwa
njia ya bahari
kwa mashua za mafunjo juu ya
maji.

Nendeni, wajumbe wepesi,
kwa taifa la watu warefu wenye
ngozi nyororo,
kwa taifa linaloogopwa mbali na
karibu,
taifa gomvi lenye lugha ngeni,
ambalo nchi yao imegawanywa
kwa mito.
3 [i]Enyi mataifa yote ya ulimwengu,
ninyi mnaoishi duniani
wakati bendera itakapoinuliwa
milimani,
mtaiona,
nayo tarumbeta itakapolia,
mtaisikia.
4 [j]Hili ndilo BWANA aliloniambia:
"Nitatulia kimya na kutazama
kutoka maskani yangu,
kama joto linalometameta katika
mwanga wa jua,
kama wingu la umande
katika joto la wakati wa mavuno."
5 [k]Kwa maana, kabla ya mavuno,
wakati wa kuchanua ukishapita
na maua yakawa zabibu zinazoiva,
atayakata machipukizi kwa mundu
wa kupogolea matawi,
naye atakata na kuyaondoa
matawi yaliyopanuka.

---

[a]**17:10** Eze 22:12; Hos 8:14; Za 68:19; Kum 6:12; Yer 2:32; Za 50:22
[b]**17:11** Za 90:6; Ay 4:8; Kum 28:39; Yer 10:19; 30:12; Law 26:30
[c]**17:12** Yer 6:23; Lk 21:25; Isa 41:11; Za 18:4; 46:6; Isa 8:7-9
[d]**17:13** Kum 28:20; Isa 13:14; Ay 13:25; Dan 2:35; Za 65:7; 46:3; Ay 21:18
[e]**17:14** 2Fal 19:35; Amu 5:31; Isa 29:5; 30:13; 33:18; 54:14
[f]**18:1** Mwa 10:6; Sef 2:12; Isa 5:8; Za 68:31; Eze 29:10; Oba 1:1
[g]1 Au: wa nzige.
[h]**18:2** Mwa 10:8-9; 2Nya 12:3; Kut 2:3; Ay 9:26; Mwa 41:14
[i]**18:3** Za 60:4; Yer 4:21; Za 33:8; Isa 5:26; 5:26; 31:9; Yos 6:21; Amu 3:27
[j]**18:4** Hos 5:15; 2Sam 1:21; Za 133:3; Isa 64:12; 26:21; Amu 5:31; Za 18:12; Isa 26:19
[k]**18:5** Isa 17:10-11; Eze 17:6; Isa 10:33

6 [a]Yote yataachwa kwa ajili ya ndege
wawindao wa mlimani
na wanyama pori,
ndege watajilisha juu yake wakati
wote wa kiangazi,
nao wanyama pori wakati wote
wa masika.

7 [b]Wakati huo matoleo yataletwa kwa
BWANA Mwenye Nguvu Zote

kutoka kwa taifa la watu warefu
wenye ngozi nyororo,
kutoka kwa taifa linaloogopwa
mbali na karibu,
kutoka taifa gomvi lenye lugha
ngeni,
ambalo nchi yao imegawanywa
kwa mito,

matoleo yataletwa katika Mlima Sayuni, mahali pa Jina la BWANA Mwenye Nguvu Zote.

*Unabii Kuhusu Misri*

19 [c]Neno kuhusu Misri:

Tazama, BWANA
amepanda juu ya wingu
liendalo kwa haraka
naye anakuja Misri.
Sanamu za Misri zinatetemeka mbele
yake,
nayo mioyo ya Wamisri inayeyuka
ndani yao.

2 [d]"Nitamchochea Mmisri dhidi ya
Mmisri,
ndugu atapigana dhidi ya ndugu,
jirani dhidi ya jirani,
mji dhidi ya mji,
ufalme dhidi ya ufalme.

3 [e]Wamisri watakufa moyo,
na nitaibatilisha mipango yao.
Watatafuta ushauri kwa sanamu na
kwa roho za waliokufa,
kwa waaguzi na kwa wale
waongeao na mizimu.
4 [f]Nitawatia Wamisri
mikononi mwa bwana mkatili
na mfalme mkali atatawala juu yao,"
asema Bwana, BWANA Mwenye
Nguvu Zote.

5 [g]Maji ya mito yatakauka,
chini ya mto kutakauka kwa jua.
6 [h]Mifereji itanuka;
vijito vya Misri vitapungua
na kukauka.
Mafunjo na nyasi vitanyauka,
7 [i]pia mimea iliyoko kando ya Mto
Naili,
pale mto unapomwaga maji
baharini.
Kila shamba lililopandwa kando ya
Mto Naili litakauka,
litapeperushwa na kutoweka
kabisa.
8 [j]Wavuvi watalia na kuomboleza,
wale wote watupao ndoano katika
Mto Naili,
watadhoofika kwa majonzi.
9 [k]Wale watu wafanyao kazi ya kitani
kilichochambuliwa watakata
tamaa,
wafumaji wa kitani safi
watavunjika moyo.
10 Wafanyao kazi ya kufuma nguo
watahuzunishwa,
nao vibarua wataugua moyoni.

---

[a]**18:6** Yer 7:33; Eze 32:4; 39:17; Isa 37:36; 8:8; 56:9
[b]**18:7** Sef 3:10; Za 68:31; 2Nya 9:24; Isa 60:7; Mwa 41:4; 41:14
[c]**19:1** Yer 43:12; Yoe 3:19; Kut 12:12; 2Sam 22:10; Yos 2:11; Isa 20:3; Kum 10:14; Isa 13:1
[d]**19:2** Amu 7:22; 12:4; Mk 13:8; Mt 10:21, 36; 24:7; 2Nya 15:6; Lk 21:10
[e]**19:3** Law 19:31; Dan 2:2, 10; Za 18:45; Ay 5:12; 2Nya 10:13; Isa 47:13
[f]**19:4** Yer 46:26; Eze 32:11; 29:19; Isa 20:4
[g]**19:5** Isa 44:27; Yer 50:38; 2Sam 14:14
[h]**19:6** Kut 7:18; Eze 30:12; Isa 37:25; 15:6; Mwa 41:2; Ay 8:11
[i]**19:7** Kum 29:23; Isa 23:3; Zek 10:11; Hes 11:5
[j]**19:8** Hes 11:5; Amo 4:2; Hab 1:15; Eze 47:10
[k]**19:9** Mit 7:16; Eze 16:10; 27:7; Yos 2:10

11 [a]Maafisa wa Soani ni wapumbavu
kabisa,
washauri wa Farao wenye busara
wanatoa ushauri wa kijinga.
Unawezaje kumwambia Farao,
“Mimi ni mmojawapo wa watu
wenye hekima,
mwanafunzi wa wafalme wa
zamani”?

12 [b]Wako wapi sasa watu wako wenye
hekima?
Wao wakuonyeshe na
kukufahamisha
ni nini BWANA Mwenye Nguvu Zote
amepanga dhidi ya Misri.
13 [c]Maafisa wa Soani wamekuwa
wapumbavu,
viongozi wa Memfisi[d]
wamedanganyika,
walio mawe ya pembe ya taifa lake
wameipotosha Misri.
14 [e]BWANA amewamwagia
roho ya kizunguzungu;
wanaifanya Misri iyumbayumbe
katika yale yote inayoyafanya,
kama vile mlevi ayumbayumbavyo
katika kutapika kwake.
15 [f]Misri haiwezi kufanya kitu
chochote,
cha kichwa wala cha mkia,
cha tawi la mtende wala cha tete.

16 [g]Katika siku ile Wamisri watakuwa
kama wanawake. Watatetemeka kwa hofu
mbele ya mkono wa BWANA Mwenye
Nguvu Zote anaoinua dhidi yao. 17 [h]Nayo
nchi ya Yuda itawatia hofu Wamisri, kila
mmoja atakayetajiwa Yuda ataingiwa na
hofu, kwa sababu ya kile ambacho BWANA
Mwenye Nguvu Zote anapanga dhidi yao.

18 [i]Katika siku hiyo miji mitano ya Misri,
itazungumza lugha ya Kanaani, na kuapa
kumtii BWANA Mwenye Nguvu Zote. Mji
mmojawapo utaitwa Mji wa Uharibifu.[j]
19 [k]Katika siku hiyo patakuwepo
madhabahu ya BWANA katikati ya Misri
na mnara wa kumbukumbu kwa BWANA
kwenye mpaka wa Misri. 20 [l]Itakuwa
alama na ushahidi kwa ajili ya BWANA
Mwenye Nguvu Zote katika nchi ya Misri.
Watakapomlilia BWANA kwa sababu ya
watesi wao, Mungu atawapelekea mwokozi
na mtetezi, naye atawaokoa. 21 [m]Hivyo
BWANA atajijulisha mwenyewe kwa
Wamisri, nao katika siku hiyo watamkubali
BWANA. Wataabudu kwa kumtolea dhabihu
na sadaka za nafaka, watamwekea BWANA
nadhiri na kuzitimiza. 22 [n]BWANA ataipiga
Misri kwa tauni; atawapiga na kuwaponya.
Watamgeukia BWANA, naye atayasikia
maombi yao na kuwaponya.
23 [o]Katika siku hiyo kutakuwepo na njia
kuu kutoka Misri hadi Ashuru. Waashuru
watakwenda Misri, na Wamisri watakwenda
Ashuru. Wamisri na Waashuru wataabudu
pamoja. 24 [p]Katika siku hiyo Israeli itakuwa
ya tatu, pamoja na Misri na Ashuru, nao
watakuwa baraka kwa dunia. 25 [q]BWANA
Mwenye Nguvu Zote atawabariki, akisema,
“Baraka iwe kwa Misri watu wangu, kwa
Ashuru kazi ya mikono yangu, na kwa
Israeli urithi wangu.”

---

[a]**19:11** Hes 13:22; 1Fal 4:30; Mdo 7:22; Mwa 41:37
[b]**19:12** 1Kor 1:20; Isa 41:22-23; Rum 9:17; Isa 14:24
[c]**19:13** Yer 2:16; Hos 9:6; Hes 13:22; Yer 46:14-19; Eze 30:13-16; Za 118:22
[d]13 Memfisi kwa Kiebrania ni Nofu.
[e]**19:14** Mit 12:8; Mt 17:17; Za 107:27
[f]**19:15** Isa 9:14
[g]**19:16** Isa 2:17; 11:10; Nah 3:13; Kum 2:25
[h]**19:17** Mwa 35:5; Isa 14:24
[i]**19:18** Za 22:27; Yer 4:2; 43:13; Isa 10:20; 24:12; 32:19; Sef 3:9; Yer 44:1; Isa 48:1
[j]18 Yaani Heliopoli (Mji wa Jua).
[k]**19:19** Yos 22:10; Kut 24:4; Za 68:18; Mwa 12:7; 28:18; Isa 10:20; Za 68:31
[l]**19:20** Isa 25:9; 49:24-26; Yos 4:20; Mwa 21:30; Amu 2:18; Kum 28:29
[m]**19:21** Isa 11:9; 43:10; 56:7; Mwa 27:29; Za 86:9; Hes 30:2; Kum 23:21
[n]**19:22** Kut 12:23; 11:10; Ebr 12:11; Eze 33:11; Yoe 2:13; Kum 32:39; Isa 45:14; Hos 10:2
[o]**19:23** Isa 11:15-16; 20:6; 27:13; 66:23; Mik 7:12; Mwa 27:29
[p]**19:24** Isa 11:11; Mwa 12:2
[q]**19:25** Za 87:4; 100:3; Efe 2:10; Kut 34:9; Yer 30:22; Hos 2:23; Mwa 12:3; Isa 29:23; 43:7

*Unabii Dhidi Ya Misri Na Kushi*

20 [a]Katika mwaka ule ambao jemadari
mkuu alitumwa na Mfalme Sargoni
wa Ashuru, naye akaja mpaka Ashdodi,
akaushambulia na kuuteka, 2 [b]wakati ule
BWANA alisema kwa kinywa cha Isaya
mwana wa Amozi. Akamwambia, “Vua
nguo ya gunia kutoka mwilini mwako
na viatu kutoka miguuni mwako.” Naye
akafanya hivyo, akatembea huku na huko
uchi, bila viatu.
3 [c]Kisha BWANA akasema, “Kama vile
mtumishi wangu Isaya alivyotembea uchi
na bila viatu kwa miaka mitatu, kama ishara
na dalili mbaya dhidi ya nchi ya Misri na
Kushi, 4 [d]vivyo hivyo mfalme wa Ashuru
atawaongoza mateka wa Wamisri, na watu
wa uhamisho wa Kushi, uchi na bila viatu,
vijana hata wazee, wakiwa matako wazi,
kwa aibu ya Wamisri. 5 [e]Wale waliotegemea
Kushi na kujivunia Misri wataogopa na
kuaibika. 6 [f]Katika siku ile watu wanaoishi
katika pwani hii watasema, ‘Tazama
lililowapata wale tuliowategemea, wale
tuliowakimbilia kwa msaada na wokovu
kutoka mikononi mwa mfalme wa Ashuru!
Tutawezaje basi kupona?’ ”

*Unabii Dhidi Ya Babeli*

21 Neno kuhusu Jangwa kando ya
Bahari:
Kama upepo wa kisulisuli unaopita
katika nchi hadi kusini,
mshambuliaji anakuja kutoka
jangwani,
kutoka nchi inayotisha.

2 [g]Nimeonyeshwa maono ya kutisha:
Msaliti anasaliti, mteka nyara
anateka nyara.
Elamu, shambulia! Umedi, izunguke
kwa jeshi!
Nitakomesha huzuni zote
alizosababisha.

3 [h]Katika hili mwili wangu umeteswa
na maumivu,
maumivu makali ya ghafula
yamenishika,
kama yale ya mwanamke mwenye
utungu wa kuzaa.
Nimeduwazwa na lile ninalolisikia,
nimeshangazwa na lile
ninaloliona.
4 [i]Moyo wangu unababaika,
woga unanifanya nitetemeke,
gizagiza la jioni nililolitamani
sana,
limekuwa hofu kuu kwangu.

5 [j]Wanaandaa meza,
wanatandaza mazulia,
wanakula, wanakunywa!
Amkeni, enyi maafisa,
zitieni ngao mafuta!

6 [k]Hili ndilo Bwana analoniambia:

“Nenda, weka mlinzi,
na atoe taarifa ya kile
anachokiona.
7 [l]Anapoona magari ya vita
pamoja na kundi la farasi,
wapanda punda au wapanda ngamia,
na awe macho, awe macho
kikamilifu.”

8 [m]Naye mlinzi alipaza sauti,

---

[a]**20:1** 2Fal 18:17; Yos 11:22; 13:3
[b]**20:2** Zek 13:4; Mt 3:4; Isa 3:24; Eze 4:1-12; 24:17, 23; 1Sam 19:24; Isa 13:1; 1Fal 1:8; Mik 1:8
[c]**20:3** Kut 3:12; Yer 7:25; Isa 8:18; 22:20; 41:8-9; Mwa 10:6; Mdo 21:11
[d]**20:4** Yer 13:22-26; Isa 19:4; 47:3; Nah 3:5; Yer 46:19; 2Sam 10:4; Ay 12:17
[e]**20:5** 2Fal 18:21; Isa 31:1-3; 8:12; 30:5; Eze 29:16
[f]**20:6** Isa 10:3; 2:11
[g]**21:2** 1Sam 24:13-16; Mwa 10:22; Za 60:3; Yer 49:34; Isa 22:6; 13:3; Yer 25:25
[h]**21:3** Mwa 3:16; Yn 16:2; Ay 14:22; Za 48:6; Isa 26:17; Yer 30:6; Dan 7:28
[i]**21:4** Isa 7:4; 35:4; 13:8; Dan 5:9; Za 55:5
[j]**21:5** Yer 25:16, 27; Dan 5:2-5; Isa 5:12; 23:7; Yer 46:3; 1Sam 1:21
[k]**21:6** 2Fal 9:17
[l]**21:7** Amu 6:5; Isa 21:9
[m]**21:8** Mik 7:7; Hab 2:1

"Mchana baada ya mchana, bwana
wangu, ninasimama katika
mnara wa ulinzi,
kila usiku ninakaa mahali pangu
nilipoamriwa.
9 [a]Tazama, yuaja mtu anayepanda gari
la vita
pamoja na kundi la farasi.
Naye anajibu:
'Babeli umeanguka, umeanguka!
Vinyago vyote vya miungu yake
vimelala chini vikiwa
vimevunjwa!' "

10 [b]Ee watu wangu, mliopondwa
kwenye sakafu ya kupuria,
ninawaambia kile nilichokisikia
kutoka kwa BWANA Mwenye Nguvu
Zote,
kutoka kwa Mungu wa Israeli.

*Unabii Dhidi Ya Edomu*

11 [c]Neno kuhusu Duma:

Mtu fulani ananiita kutoka Seiri,
"Mlinzi, usiku utaisha lini?
Mlinzi, usiku utaisha lini?"
12 Mlinzi anajibu,
"Asubuhi inakuja, lakini pia usiku.
Kama ungeliuliza, basi uliza;
bado na urudi tena."

*Unabii Dhidi Ya Arabia*

13 [d]Neno kuhusu Arabia:

Enyi misafara ya Wadedani,
mnaopiga kambi katika vichaka
vya Arabia,
14 [e]leteni maji kwa wenye kiu,
ninyi mnaoishi Tema,
leteni chakula kwa ajili ya
wakimbizi.
15 [f]Wanaukimbia upanga,
kutoka upanga uliochomolewa
alani,
kutoka upinde uliopindwa,
na kutoka kwenye joto la vita.

16 [g]Hili ndilo Bwana analoniambia:
"Katika muda wa mwaka mmoja, kama
vile mtumishi aliyefungwa na mkataba
angeihesabu, majivuno yote ya Kedari
yatafikia mwisho. 17 [h]Wanaume wavutao
pinde walionusurika, mashujaa wa Kedari,
watakuwa wachache." BWANA, Mungu wa
Israeli, amesema.

*Unabii Kuhusu Yerusalemu*

22 [i]Neno kuhusu Bonde la Maono:

Nini
kinachokutaabisha sasa,
kwamba ninyi nyote mmepanda
juu ya mapaa?
2 [j]Ewe mji uliojaa ghasia,
ewe mji wa makelele na sherehe!
Watu wenu waliokufa hawakuuawa
kwa upanga,
wala hawakufa vitani.
3 [k]Viongozi wako wote wamekimbia
pamoja,
wamekamatwa bila kutumia
upinde.
Ninyi nyote mliokamatwa
mlichukuliwa wafungwa
pamoja,
mlikimbia wakati adui alipokuwa
bado mbali.

---

[a] **21:9** Isa 13:19; Ufu 14:8; Dan 5:30; Ufu 18:2; Yer 50:2; Isa 47:11; Yer 51:8
[b] **21:10** Yer 51:33; Mt 3:12; Mik 4:13; Isa 27:12; Hab 3:12
[c] **21:11** Mwa 32:3; 1Nya 1:30; Eze 35:2; Oba 1:1
[d] **21:13** Isa 13:1; 2Nya 9:14; Mwa 10:7; 25:3; 1Nya 1:9
[e] **21:14** Mwa 25:15; Ay 6:19
[f] **21:15** Isa 13:14; 31:8
[g] **21:16** Law 25:50; Mwa 25:13; 25:13; Isa 17:3; 16:14; Za 120:5; Law 25:50; Wim 1:5; Mwa 25:13
[h] **21:17** Hes 23:19; Kum 4:27; Isa 10; 19; 1:20; 16:14; Lk 21:33; 1Sam 15:29; Mt 24:35; Mk 13:31; 1Pet 1:25
[i] **22:1** Za 125:2; Yoe 3:2-14; Yos 2:8; Isa 13:1; Yer 48:38; 21:13
[j] **22:2** Isa 5:14; 32:13; Eze 22:5; Isa 21:5; 10:4; 2Fal 25:3
[k] **22:3** Isa 13:14; 2Fal 25:6

4 [a]Kwa hiyo nilisema, "Geukia mbali nami,
niache nilie kwa uchungu.
Usijaribu kunifariji
juu ya maangamizi ya watu wangu."

5 [b]Bwana, BWANA Mwenye Nguvu Zote, anayo siku
ya ghasia, ya kukanyaga, na ya kuogofya
katika Bonde la Maono,
siku ya kuangusha kuta
na ya kupiga kelele mpaka milimani.
6 [c]Elamu analichukua podo,
pamoja na waendesha magari ya vita na farasi.
Kiri anaifungua ngao.
7 [d]Mabonde yako yaliyo mazuri sana
yamejaa magari ya vita,
nao wapanda farasi wamewekwa
kwenye malango ya mji;
8 [e]ulinzi wa Yuda umeondolewa.

Nawe ulitazama siku ile
silaha katika Jumba la Kifalme la Mwituni,
9 [f]mkaona kuwa Mji wa Daudi
una matundu mengi katika ulinzi wake,
mkaweka akiba ya maji
kwenye Bwawa la Chini.
10 [g]Mlihesabu majengo katika Yerusalemu
nanyi mkabomoa nyumba ili kuimarisha ukuta.
11 [h]Mlijenga bwawa la maji katikati ya kuta mbili
kwa ajili ya maji ya Bwawa la Zamani,
lakini hamkumtazama Yule aliyelitengeneza,
au kuwa na heshima kwa Yule
aliyeubuni tangu zamani za kale.

12 [i]Bwana, BWANA Mwenye Nguvu Zote,
aliwaita siku ile
ili kulia na kuomboleza,
kung'oa nywele zenu na kuvaa nguo ya gunia.
13 [j]Lakini tazama, kuna furaha na sherehe,
kuchinja ng'ombe na kuchinja kondoo,
kula nyama na kunywa mvinyo!
Mnasema, "Tuleni na kunywa,
kwa kuwa kesho tutakufa!"

14 [k]BWANA Mwenye Nguvu Zote amelifunua hili nikiwa ninasikia: Bwana, BWANA Mwenye Nguvu Zote, asema: "Mpaka siku ya kufa kwenu, dhambi hii haitafanyiwa upatanisho."

15 [l]Hili ndilo Bwana, BWANA Mwenye Nguvu Zote, asemalo:

"Nenda ukamwambie huyu wakili Shebna,
ambaye ni msimamizi wa jumba la kifalme:
16 [m]Unafanya nini hapa, na ni nani aliyekupa ruhusa
kujikatia kaburi lako mwenyewe,

[a]**22:4** Mao 1:16; Lk 19:41; Yer 9:1; Eze 21:6; Isa 15:3; Lk 19:41
[b]**22:5** Amo 5:18-20; Es 3:15; Sef 1:15; Isa 2:12; Ay 40:12; 2Sam 22:43; Eze 8:17-18; 13:14; Mao 1:5
[c]**22:6** Isa 21:2; 2Fal 16:9; Yer 51:56; 49:35; Za 46:9
[d]**22:7** Yos 15:18; 2Nya 32:1-2
[e]**22:8** 2Nya 32:5; 1Fal 7:2; Isa 2:12
[f]**22:9** 2Fal 18:17; 2Nya 32:4-5; Wim 4:4; 2Fal 20:20
[g]**22:10** Yer 33:4; 2Nya 32:15; 32:5; Yer 33:4
[h]**22:11** Yer 39:4; Neh 3:16; 2Fal 25:4; 19:25; 1Sam 12:24
[i]**22:12** Yoe 2:17; Law 13:40; Mik 1:16; Isa 3:24; Yoe 1:9-13
[j]**22:13** Mhu 8:15; Isa 5:12; 21:5; Lk 17:26-29; 1Kor 15:32; 1Sam 25:36; Isa 28:7-8
[k]**22:14** Eze 24:13; Isa 5:9; 1Sam 2:25; Isa 13:11; 30:13-14; 1Sam 3:14
[l]**22:15** 2Fal 6:30; 18:18; Mwa 41:40; Isa 36:3; 1Fal 4:6
[m]**22:16** Mt 27:60; Hes 32:42

ukichonga kaburi lako mahali palipo
juu,
na kutoboa kwa patasi mahali
pako pa kupumzikia katika
mwamba?

17 [a]"Jihadhari, BWANA yu karibu
kukukamata thabiti,
na kukutupa mbali, ewe mtu
mwenye nguvu.
18 [b]Atakuvingirisha uwe kama mpira
na kukutupa katika nchi kubwa.
Huko ndiko utakakofia,
na huko ndiko magari yako ya vita
ya fahari yatabakia,
wewe unayeifedhehesha nyumba
ya bwana wako!
19 [c]Nitakuondoa kutoka kazi yako,
nawe utaondoshwa kutoka nafasi
yako.

20 [d]"Katika siku ile, nitamwita mtumishi
wangu, Eliakimu mwana wa Hilkia.
21 [e]Nitamvika joho lako, nami nitamfunga
mshipi wako kiunoni mwake, na kumkabidhi
mamlaka yako. Yeye atakuwa baba kwa
wale wanaoishi Yerusalemu na kwa
nyumba ya Yuda. 22 [f]Nitaweka mabegani
mwake ufunguo wa nyumba ya Daudi. Kile
afunguacho hakuna awezaye kufunga, na
kile afungacho hakuna awezaye kufungua.
23 [g]Nitamgongomea kama kigingi kilicho
mahali palipo imara, naye atakuwa kiti cha
enzi cha heshima kwa ajili ya nyumba ya
baba yake. 24 Utukufu wote wa jamaa yake
utakuwa juu yake: Watoto wa jamaa hiyo
na machipukizi yake, vyombo vyake vyote
vidogo, tangu bakuli hadi magudulia yote."
25 [h]BWANA Mwenye Nguvu Zote asema,
"Katika siku ile, kigingi kilichogongomewa
mahali imara kitaachia njia. Kitakatwa,
nacho kitaanguka na mzigo ulioning'inia juu
yake utaanguka chini." BWANA amesema.

*Unabii Kuhusu Tiro*

23 [i]Neno kuhusu Tiro:

Ombolezeni, enyi meli
za Tarshishi!
Kwa kuwa Tiro imeangamizwa,
imeachwa bila nyumba wala
bandari.
Kuanzia nchi ya Kitimu[j]
neno limewajia.

2 [k]Nyamazeni kimya, enyi watu wa
kisiwani,
pia ninyi wafanyabiashara wa
Sidoni,
ambao mabaharia
wamewatajirisha.
3 [l]Kwenye maji makuu
nafaka za Shihori zilikuja;
mavuno ya Naili yalikuwa mapato
ya Tiro,
naye akawa soko la mataifa.

4 [m]Uaibishwe ee Sidoni, nawe ee
ngome la bahari,
kwa kuwa bahari imesema:
"Sijapata kuwa na uchungu wa
kuzaa wala sijapata kuzaa,
wala sijapata kulea wana wala
kutunza mabinti."
5 [n]Habari ifikapo Misri,
watakuwa katika maumivu makuu
kwa ajili ya taarifa kutoka
Tiro.

6 [o]Vukeni mpaka Tarshishi,
ombolezeni, enyi watu wa
kisiwani.

---

[a]**22:17** Yer 10:18; 13:18; 22:26
[b]**22:18** Ay 18:11; Isa 14:19; Mwa 41:43
[c]**22:19** Za 52:5; Lk 16:3
[d]**22:20** 2Fal 18:18
[e]**22:21** Ay 29:16
[f]**22:22** 1Nya 9:27; Mt 16:19; Ay 12:14; Ufu 3:7; Isa 7:2
[g]**22:23** Eze 15:3; Zek 10:4; Ezr 9:8; Ay 6:25; 1Sam 2:7-8; Ay 36:7
[h]**22:25** Isa 46:11; Mik 4:4
[i]**23:1** Zek 9:2-4; Amo 1:9-10; Eze 26:1-21; Mwa 10:4; 1Fal 10:22; Yos 19:29; Yer 47:4
[j]1 Kitimu hapa ni Kipro, kisiwa katika Bahari ya Mediterania.
[k]**23:2** Ay 2:13; Eze 27:1-24; Amu 1:31
[l]**23:3** Isa 19:7; Za 83:7; Eze 27:3; Mwa 41:5
[m]**23:4** Mwa 10:15, 19
[n]**23:5** Eze 30:9; 26:17-18
[o]**23:6** Mwa 10:4

7 [a]Je, huu ndio mji wenu uliojaa
sherehe,
mji wa zamani, zamani kabisa
ambao miguu yake imeuchukua
kufanya makao nchi za mbali
sana?
8 [b]Ni nani amepanga hili dhidi ya Tiro,
mji utoao mataji,
ambao wafanyabiashara wake ni
wana wa mfalme
na wachuuzi wake ni watu
mashuhuri wa dunia?
9 [c]Bwana Mwenye Nguvu Zote ndiye
alipanga jambo hili,
ili kukishusha kiburi cha utukufu
wote
na kuwanyenyekesha wale wote
ambao ni mashuhuri duniani.

10 Ee Binti Tarshishi,
pita katika nchi yako kama vile
Mto Naili
kwa kuwa huna tena bandari.
11 [d]Bwana amenyoosha mkono wake
juu ya bahari
na kuzifanya falme zake
zitetemeke.
Ametoa amri kuhusu Kanaani
kwamba ngome zake
ziangamizwe.
12 [e]Alisema, "Usizidi kufurahi,
ee Bikira Binti Sidoni, sasa
umepondwa!

"Simama, vuka uende Kitimu;
hata huko hutapata pumziko."
13 [f]Tazama katika nchi ya Wakaldayo,
watu hawa ambao sasa
hawaonekani kama wapo!
Waashuru wameifanya nchi hiyo
kuwa mahali pa viumbe wa
jangwani.
Wamesimamisha minara yao ya vita
kuuzunguka,
wameziteka ngome zake na
kuziacha tupu
na kuufanya kuwa magofu.

14 [g]Ombolezeni, enyi meli za Tarshishi;
ngome yenu imeangamizwa!

15 [h]Wakati huo Tiro utasahauliwa kwa
miaka sabini, muda wa maisha ya mfalme.
Lakini mwisho wa miaka hiyo sabini,
itakuwa kwa Tiro kama ilivyo katika wimbo
wa kahaba:

16 [i]"Twaa kinubi, tembea mjini kote,
ewe kahaba uliyesahauliwa;
piga kinubi vizuri, imba nyimbo
nyingi,
ili upate kukumbukwa."

17 [j]Mwishoni mwa miaka sabini, Bwana
atashughulika na Tiro. Naye atarudia ajira
yake ya ukahaba, na atafanya biashara
yake na falme zote juu ya uso wa dunia.
18 [k]Lakini faida na mapato yake yatawekwa
wakfu kwa Bwana; hayatahifadhiwa wala
kufichwa. Faida zake zitakwenda kwa
wale wakaao mbele za Bwana kwa ajili
ya chakula tele na mavazi mazuri.

### *Dunia Kuharibiwa Upesi*

24 [l]Tazama, Bwana ataifanya dunia
kuwa ukiwa
na kuiharibu,
naye atauharibu uso wake
na kutawanya wakaao ndani yake:

---

[a]**23:7** Isa 5:14; 32:13; 22:2; Eze 26:13; Isa 23:12
[b]**23:8** Isa 2:12; Eze 28:2; 1Tim 3:4; Nah 3:16; Eze 28:5; Ufu 18:23
[c]**23:9** Ay 40:11; Isa 13:11; 5:13; Eze 27:3; Isa 14:24; 9:15
[d]**23:11** Kut 14:21; Eze 26:4; Zek 9:3-4; Za 46:6
[e]**23:12** Ufu 18:22; Sef 3:14; Zek 2:10; Isa 37:22; Yer 14:17; Mao 2:13; Mwa 10:4
[f]**23:13** Isa 43:14; Yer 51:12; Za 74:14; Isa 18:6
[g]**23:14** Mwa 10:4; Isa 2:16; Eze 27:25; 1Fal 10:22
[h]**23:15** Yer 25:22; Za 90:10
[i]**23:16** Mit 7:10
[j]**23:17** Kum 23:17-18; Mwa 10:15-19; Ufu 17:1; 18:3-9; Eze 16:26; Yer 25:26; Nah 3:4
[k]**23:18** Yos 6:17-19; Za 72:10; Zek 14:20-21; Isa 61:6; Mik 4:13; Kut 28:36; Isa 18:7; 60:5-9; Amo 1:9-10
[l]**24:1** Isa 2:19-21; Yer 25:29; Yos 6:17; Isa 13:5; 33:9; Mwa 11:9

2 [a]ndivyo itakavyokuwa
kwa makuhani na kwa watu,
kwa bwana na kwa mtumishi,
kwa bibi na kwa mtumishi wake
wa kike,
kwa muuzaji na kwa mnunuzi,
kwa mkopaji na kwa mkopeshaji,
kwa mdaiwa na kwa mdai.
3 [b]Dunia itaharibiwa kabisa
na kutekwa nyara kabisa.
BWANA amesema neno hili.

4 [c]Dunia inakauka na kunyauka,
dunia inanyong'onyea na
kunyauka,
waliotukuzwa wa dunia
wananyong'onyea.
5 [d]Dunia imetiwa unajisi na watu
wake;
wameacha kutii sheria,
wamevunja amri
na kuvunja agano la milele.
6 [ef]Kwa hiyo laana inaiteketeza dunia,
watu wake lazima waichukue
hatia yao.
Kwa hiyo wakazi wa dunia
wameteketezwa,
nao waliosalia ni wachache sana.
7 [g]Divai mpya inakauka na mzabibu
unanyauka,
watu wote wafurahishao wanalia
kwa huzuni.
8 [h]Furaha ya matoazi imekoma,
kelele za wenye furaha zimekoma,
shangwe za kinubi zimenyamaza.
9 [i]Hawanywi tena mvinyo pamoja na
wimbo,
kileo ni kichungu kwa wanywaji
wake.
10 [j]Mji ulioharibiwa umekuwa ukiwa,
mlango wa kila nyumba
umefungwa.
11 [k]Barabarani wanalilia kupata
mvinyo,
furaha yote imegeuka kuwa
majonzi,
furaha yote imefukuziwa mbali na
dunia.
12 [l]Mji umeachwa katika uharibifu,
lango lake limevunjwa vipande.
13 [m]Ndivyo itakavyokuwa duniani
na miongoni mwa mataifa,
kama vile wakati mzeituni
upigwavyo,
au kama vile wakati masazo
yabakiavyo baada ya zabibu
kuvunwa.

14 [n]Wanainua sauti zao, wanapiga
kelele kwa furaha,
kutoka magharibi wanasifu kwa
ukelele utukufu wa BWANA.
15 [o]Kwa hiyo upande wa mashariki
mpeni BWANA utukufu,
liadhimisheni jina la BWANA,
Mungu wa Israeli,
katika visiwa vya bahari.
16 [p]Kutoka miisho ya dunia tunasikia
uimbaji:
"Utukufu kwa Yule Mwenye
Haki."

Lakini nilisema, "Ninadhoofika,
ninadhoofika!
Ole wangu!

---

[a]**24:2** Eze 7:12; Hos 4:9; 1Kor 7:29-31; Law 25:35-37; Kum 23:19-20; Law 25:35-37; Isa 3:1-7
[b]**24:3** Isa 6:11-12; 10:6; 7:7; Mwa 6:13
[c]**24:4** Yos 12:11; Yer 14:4; Isa 15:6; 1Sam 2:12; Yoe 1:10
[d]**24:5** Mwa 3:17; Hes 35:33; Law 18:25; Isa 59:12; 9:17; Yer 7:28; 11:10; Mwa 9:11
[e]**24:6** Yer 50:15; Isa 20:6
[f]**24:6** Kum 28:15; Law 26:15; Dan 9:11; Yos 23:15
[g]**24:7** Isa 32:10; 7:23; Yoe 1:10-12; Isa 16:8-10
[h]**24:8** Mwa 31:27; Isa 5:14; Mao 5:14; Eze 26:13; Yer 7:34; 16:9; Ufu 5:14
[i]**24:9** Isa 5:11, 20-22
[j]**24:10** Isa 25:2; 26:5; 6:11
[k]**24:11** Isa 15:6; 16:10; 32:13; Yer 14:3; Za 144:14; Mao 2:12
[l]**24:12** Isa 19:18; 3:26; 13:2
[m]**24:13** Kum 30:4; Isa 17:6; Mik 7:1
[n]**24:14** Isa 12:6; 43:5; 49:12
[o]**24:15** Isa 45:12; 2The 1:12; Mal 1:11; Kut 15:2; Za 113:3; Isa 25:3; 12:4; 59:19
[p]**24:16** Isa 28:5; Yer 3:20; 9:2; 10:19; Za 48:10; Hos 5:7; Ezr 9:15; 1Sam 4:8

Watenda hila wanasaliti!
Kwa hila watenda hila wanasaliti!”
17 [a]Hofu, shimo na mtego
vinakungojea,
ewe mtu ukaaye duniani.
18 [b]Kila akimbiaye asikiapo sauti ya
hofu
atatumbukia shimoni,
naye yeyote apandaye kutoka
shimoni,
atanaswa kwenye mtego.

Malango ya gharika ya mbinguni
yamefunguliwa,
misingi ya dunia inatikisika.
19 [c]Dunia imepasuka,
dunia imechanika,
dunia imetikiswa kabisa.
20 [d]Dunia inapepesuka kama mlevi,
inayumbayumba kama kibanda
kwenye upepo;
imelemewa sana na mzigo wa hatia
ya uasi wake
na ikianguka kamwe haitainuka
tena.

21 [e]Katika siku ile BWANA ataadhibu
nguvu zilizoko mbinguni juu,
na wafalme walioko duniani chini.
22 [f]Watakusanywa pamoja
kama wafungwa waliofungwa
gerezani,
watafungiwa gerezani
na kuadhibiwa baada ya siku
nyingi.
23 [g]Mwezi utatiwa haya, nalo jua
litaaibishwa;
kwa maana BWANA Mwenye
Nguvu Zote atawala
juu ya Mlima Sayuni na katika
Yerusalemu,
tena mbele ya wazee wake kwa
utukufu.

*Msifuni* BWANA

25 [h]Ee BWANA, wewe ni Mungu
wangu,
nitakutukuza na kulisifu jina lako,
kwa maana katika ukamilifu wa
uaminifu
umetenda mambo ya ajabu,
mambo yaliyokusudiwa tangu
zamani.
2 [i]Umeufanya mji kuwa lundo la
kifusi,
mji wenye ngome kuwa magofu,
ngome imara ya wageni kuwa si mji
tena,
wala hautajengwa tena kamwe.
3 [j]Kwa hiyo mataifa yenye nguvu
yatakuheshimu,
miji ya mataifa katili
itakuheshimu wewe.
4 [k]Umekuwa kimbilio la watu maskini,
kimbilio la mhitaji katika taabu
yake,
hifadhi wakati wa dhoruba
na kivuli wakati wa hari.
Kwa maana pumzi ya wakatili
ni kama dhoruba ipigayo ukuta
5 [l]na kama joto la jangwani.
Wewe wanyamazisha makelele ya
wageni;
kama vile hari ipunguzwavyo na
kivuli cha wingu,
ndivyo wimbo wa wakatili
unyamazishwavyo.

---

[a]**24:17** Isa 8:14; Yer 48:43; Amo 5:19; Kum 32:23-25; Lk 21:35
[b]**24:18** Mwa 7:11; Amu 5:4; Ay 18:19; 20:24; Za 18:7; Isa 42:22; Mao 3:47; Eze 38:15
[c]**24:19** Yer 4:23; Kum 11:6; Za 46:2
[d]**24:20** Ay 12:15; 27:18; Isa 1:2, 28; 19:14; 43:27; Za 46:2; Isa 58:1; Ay 12:14, 25
[e]**24:21** Isa 13:11; 2:11; Yer 25:29; Za 76:12; Isa 10:20; Ufu 16:14; 1Kor 6:3; Efe 6:12
[f]**24:22** Isa 42:7, 22; Lk 8:31; Eze 38:8; Isa 10:4; Ufu 20:7-10
[g]**24:23** Za 97:1; Ufu 22:5; Ebr 12:22; Ufu 21:23; Isa 13:10; 28:5; 41:16
[h]**25:1** Hes 23:19; Za 40:5; Yoe 2:21-26; Isa 7:13; 14:24; 37:26; Efe 1:11
[i]**25:2** Isa 37:26; Yer 51:37; Isa 17:3; 13:22; Kum 13:16; Ay 12:14
[j]**25:3** Kut 6:2; Za 22:23; Isa 11:14; 13:11; Ufu 11:13
[k]**25:4** Yoe 3:16; Isa 33:16; Za 46:1-11; Isa 49:25; 2Sam 22:3; Za 118:8; Isa 3:14
[l]**25:5** Yer 51:25; Za 18:44; Isa 13:11

6 [a]Juu ya mlima huu BWANA Mwenye Nguvu Zote ataandaa
karamu ya vinono kwa mataifa yote,
karamu ya mvinyo wa zamani,
nyama nzuri sana na divai zilizo bora sana.
7 [b]Juu ya mlima huu ataharibu
sitara ihifadhiyo mataifa yote,
kile kifuniko kifunikacho mataifa yote,
8 [c]yeye atameza mauti milele.
BWANA Mwenyezi atafuta machozi katika nyuso zote;
ataondoa aibu ya watu wake duniani kote.
BWANA amesema hili.

9 [d]Katika siku ile watasema,
"Hakika huyu ndiye Mungu wetu;
tulimtumaini, naye akatuokoa.
Huyu ndiye BWANA, tuliyemtumaini;
sisi tushangilie na kufurahia katika wokovu wake."

10 [e]Mkono wa BWANA utatulia juu ya mlima huu,
bali Moabu atakanyagwa chini
kama majani makavu yakanyagwavyo kwenye shimo la mbolea.
11 [f]Watakunjua mikono yao katikati yake,
kama vile mwogeleaji akunjuavyo mikono yake ili aogelee.
Mungu atashusha kiburi chao
licha ya ujanja wa mikono yao.
12 [g]Atabomoa kuta ndefu za maboma yako
na kuziangusha chini,
atazishusha chini ardhini,
mpaka mavumbini kabisa.

*Wimbo Wa Ushindi*

26 [h]Katika siku ile, wimbo huu utaimbwa katika nchi ya Yuda:

Tuna mji ulio na nguvu,
Mungu huufanya wokovu kuwa kuta zake na maboma yake.
2 [i]Fungua malango ili taifa lenye haki lipate kuingia,
taifa lile lidumishalo imani.
3 [j]Utamlinda katika amani kamilifu
yeye ambaye moyo wake ni thabiti
kwa sababu anakutumaini wewe.
4 [k]Mtumaini BWANA milele,
kwa kuwa BWANA, BWANA, ni Mwamba wa milele.
5 [l]Huwashusha wale wajikwezao,
huushusha chini mji wenye kiburi,
huushusha hadi ardhini
na kuutupa chini mavumbini.
6 [m]Miguu huukanyaga chini,
miguu ya hao walioonewa,
hatua za hao maskini.

7 [n]Mapito ya wenye haki yamenyooka.
Ewe uliye Mwenye Haki,
waisawazisha njia ya mtu mnyofu.
8 [o]Naam, BWANA, tukienenda katika sheria zako,
twakungojea wewe,
jina lako na sifa zako
ndizo shauku za mioyo yetu.

---

[a]**25:6** Mt 22:4; Mit 9:2; Dan 7:14; Mwa 29:22; Za 36:8
[b]**25:7** 2Kor 3:15-16; Efe 4:8; 1:17; Ay 4:9
[c]**25:8** Hos 13:14; 1Kor 15:54-55; Yer 31:16; Ufu 7:14-17; Ebr 2:14; Isa 26:19
[d]**25:9** Isa 40:9; Yer 14:8; Za 20:5; Kum 32:43; Isa 2:11; 49:25-26; Za 145:19
[e]**25:10** Mwa 19:37; Hes 21:29; Kum 23:6; Isa 11:14; Amo 2:1-2
[f]**25:11** Isa 5:25; 14:26; Law 26:19; Ay 40:12; Isa 2:10-17; 16:14
[g]**25:12** Ay 40:11; Isa 26:5; Yer 51:44; Isa 2:15
[h]**26:1** Isa 14:32; Zek 2:5; Isa 10:20; 30:29; 32:18; Zek 9:8; Za 48:13
[i]**26:2** Isa 58:8; 62:2; Ufu 21:13; Za 24:4-7; 83:13; Isa 1:26; 50:8
[j]**26:3** Ay 22:21; Flp 4:7; Isa 9:6-7; 1Nya 5:20; Za 28:7; 22:5
[k]**26:4** Isa 12:2; 50:10; Za 62:8; Mwa 49:24
[l]**26:5** Isa 25:12; 25:5; Eze 26:11
[m]**26:6** Isa 5:5; 49:26; 3:15; 14:30
[n]**26:7** Kum 32:4; Kut 14:19; Isa 42:16; Za 26:12; 25:8; Isa 40:4
[o]**26:8** Za 18:22; 145:2; Isa 12:4; Kum 18:18; Isa 65:5; Za 37:9

9 [a]Nafsi yangu yakutamani wakati wa usiku,
wakati wa asubuhi roho yangu yakuonea shauku.
Wakati hukumu zako zinapokuja juu ya dunia,
watu wa ulimwengu hujifunza haki.
10 [b]Ingawa neema yaonyeshwa kwa waovu,
hawajifunzi haki,
hata katika nchi ya unyofu huendelea kutenda mabaya
wala hawazingatii utukufu wa BWANA.
11 [c]Ee BWANA, mkono wako umeinuliwa juu,
lakini hawauoni.
Wao na waone wivu wako kwa ajili ya watu wako tena waaibishwe,
moto uliowekwa akiba kwa ajili ya adui zako na uwateketeze.

12 [d]BWANA, unaamuru amani kwa ajili yetu,
yale yote tuliyoweza kuyakamilisha ni wewe uliyetenda kwa ajili yetu.
13 [e]Ee BWANA, Mungu wetu, mabwana wengine zaidi ya wewe wametutawala,
lakini jina lako pekee ndilo tunaloliheshimu.
14 [f]Wao sasa wamekufa, wala hawako tena hai,
roho za waliokufa hazitarudi tena.
Uliwaadhibu na kuwaangamiza,
umefuta kumbukumbu lao lote.
15 [g]Umeliongeza hilo taifa, Ee BWANA,
umeliongeza hilo taifa.
Umejipatia utukufu kwa ajili yako mwenyewe,
umepanua mipaka yote ya nchi.

16 [h]BWANA, walikujia katika taabu yao,
wewe ulipowarudi,
waliweza kuomba kwa kunong'ona tu.
17 [i]Kama mwanamke mwenye mimba aliyekaribia kuzaa
anavyogaagaa na kulia kwa ajili ya maumivu yake,
ndivyo tulivyokuwa mbele zako, Ee BWANA.
18 [j]Tulikuwa na mimba, tuligaagaa kwa maumivu,
lakini tulizaa upepo.
Hatukuleta wokovu duniani,
hatujazaa watu katika ulimwengu huu.

19 [k]Lakini wafu wenu wataishi,
nayo miili yao itafufuka.
Ninyi mnaokaa katika mavumbi,
amkeni mkapige kelele kwa furaha.
Umande wenu ni kama umande wa asubuhi,
dunia itawazaa wafu wake.

20 [l]Nendeni, watu wangu, ingieni vyumbani mwenu
na mfunge milango nyuma yenu,
jificheni kwa kitambo kidogo
mpaka ghadhabu yake ipite.
21 [m]Tazama, BWANA anakuja kutoka makao yake
ili kuwaadhibu watu wa dunia kwa ajili ya dhambi zao.

---

[a]**26:9** Za 42:1-2; Mt 6:33; Za 63:6; 119:55; 1Nya 16:14; Za 78:34
[b]**26:10** Isa 32:6; 1Sam 12:24; Rum 2:4; Mhu 8:12; Mt 5:45; Isa 22:12-13; Yer 2:19; Yn 5:38
[c]**26:11** Ay 34:27; Isa 18:3; 44:9, 18; Ebr 10:27; Za 10:12; Yoe 2:18; Zek 1:14; Mik 7:16
[d]**26:12** Za 119:165; Isa 9:6; Za 68:28
[e]**26:13** Za 66:12; Isa 42:8; 2:8; 63:7
[f]**26:14** Kum 4:28; Za 9:5; Isa 10:3; Ay 28:5
[g]**26:15** Isa 33:17; 14:2; Ay 12:23
[h]**26:16** Amu 6:2; Hos 5:15; Isa 5:30; Za 39:11; Isa 29:4
[i]**26:17** Isa 21:3; Ufu 12:2; Yn 16:21
[j]**26:18** Isa 59:4; Mwa 49:10; Za 17:14; Isa 42:6; 49:6; 51:4; Yer 12:16
[k]**26:19** Hos 13:14; Efe 5:14; Isa 25:8; Eze 37:1-14; Dan 12:2; Isa 18:4; Mwa 27:28; Za 22:29
[l]**26:20** Kut 12:23; Za 30:5; Ay 14:13; 2Kor 4:17; Isa 10:25; 30:27
[m]**26:21** Yud 14; Mik 1:3; Ay 16:18; Isa 29:6; 18:4; Lk 11:50-51; Isa 30:12-14

Dunia itadhihirisha umwagaji damu
juu yake,
wala haitaendelea kuwaficha watu
wake waliouawa.

*Wokovu Kwa Ajili Ya Israeli*

27 [a]Katika siku ile,
BWANA ataadhibu kwa
upanga wake,
upanga wake mkali, mkubwa na
wenye nguvu,
ataadhibu Lewiathani[b] yule nyoka
apitaye kwa mwendo laini,
Lewiathani yule nyoka mwenye
kujipinda;
atamuua joka huyo mkubwa sana wa
baharini.

2 [c]Katika siku ile:

"Imbeni kuhusu shamba la mizabibu
lililozaa:
3 [d]Mimi, BWANA, ninalitunza,
nalinyweshea maji mfululizo.
Ninalichunga usiku na mchana
ili mtu yeyote asije akalidhuru.
4 [e]Mimi sijakasirika.
Licha pangekuwepo michongoma
na miiba kunikabili!
Ningepambana dhidi yake katika
vita,
ningeliichoma moto yote.
5 [f]Au niwaache waje kwangu kwa ajili
ya kupata kimbilio,
wao na wafanye amani nami,
naam, wafanye amani nami."

6 [g]Katika siku zijazo, Yakobo atatia
mizizi,
Israeli atatoa chipukizi na
kuchanua maua,
naye atajaza ulimwengu wote kwa
matunda.

7 [h]Je, BWANA amempiga
vile alivyowapiga wale
waliompiga?
Je, yeye ameuawa
vile walivyouawa wale waliomuua
yeye?
8 [i]Kwa vita na kwa kumfukuza
unapingana naye:
kwa mshindo wake mkali
anamfukuza,
kama siku ile uvumapo upepo wa
mashariki.
9 [j]Kwa hili, basi, hatia ya Yakobo
itafanyiwa upatanisho,
nalo hili litakuwa matunda ya
utimilizo wa kuondolewa kwa
dhambi yake:
Wakati atakapoyafanya mawe yote
ya madhabahu
kuwa kama mawe ya chokaa
yaliyopondwa vipande
vipande,
hakuna nguzo za Ashera au
madhabahu za kufukizia
uvumba
zitakazobaki zimesimama.
10 [k]Mji ulio na boma umebaki ukiwa,
makao yaliyotelekezwa,
yaliyoachwa kama jangwa.
Huko ndama hulisha,
huko hujilaza,
wanakwanyua matawi yake.

---

[a]**27:1** Eze 29:3; Mwa 3:24; Hes 3:15; Ufu 12:9; Isa 2:11; Kum 32:41; Ay 26:13; Za 68:30; Isa 28:5; 31:8; 34:6; 66:16; Eze 21:3; Ay 3:8
[b]1 Lewiathani ni mnyama mkubwa wa baharini mwenye magamba anayefanana na joka kubwa, mwenye umbo la kutisha, asiyeweza kuvuliwa.
[c]**27:2** Yer 2:21; Isa 24:21; 5:1
[d]**27:3** Isa 58:11; Za 91:4; Yn 6:39; Isa 5:2
[e]**27:4** Isa 10:17; Mt 3:12; 2Sam 23:6; Ebr 6:8
[f]**27:5** Isa 25:4; Efe 2:12-14; Ay 22:21; Za 119:165; Rum 5:1; 2Kor 5:20
[g]**27:6** Mwa 40:10; Hos 14:5-8; Za 72:16; 2Fal 19:30; Eze 17:23; 36:8; Isa 11:1
[h]**27:7** Isa 10:26; 37:36-38
[i]**27:8** Isa 49:14; Yer 10:24; Ay 23:6; Isa 54:7; Mwa 41:6; Isa 50:1
[j]**27:9** Kut 34:13; Rum 11:27; Za 78:38; Kut 23:24; 2Nya 14:5; Law 26:30
[k]**27:10** Kum 13:16; Isa 17:2; 5:5, 17; Mao 5:18; Yer 26:6; 10:22; Isa 32:14; Mwa 1:2; Kum 13:16; Isa 5:6; 32:14; Yer 10:22; Law 1:4; 5:18; Isa 5:5; 5:17; 17:2

11 [a]Wakati vijiti vyake vimekauka,
huvunjwa
nao wanawake huja na kuwasha
navyo moto.
Kwa kuwa hili ni taifa lisilo na
ufahamu,
kwa hiyo yeye aliyewafanya hana
huruma juu yao,
Muumba wao hawaonyeshi
fadhili.

12 [b]Katika siku ile BWANA atapura kutoka
matiririko ya Mto Frati hadi Kijito cha
Misri, nanyi ee Waisraeli, mtakusanywa
mmoja mmoja. 13 [c]Katika siku ile tarumbeta
kubwa italia. Wale waliokuwa wakiangamia
katika nchi ya Ashuru, nao wale waliokuwa
uhamishoni katika nchi ya Misri watakuja
na kumwabudu BWANA katika mlima
mtakatifu huko Yerusalemu.

*Ole Wa Efraimu*

28 [d]Ole kwa lile taji la maua, kiburi
cha walevi wa Efraimu,
kwa ua linalosinyaa, uzuri wa
utukufu wake,
uliowekwa kwenye kichwa cha
bonde lenye rutuba:
kwa ule mji, kiburi cha wale
walioshushwa na mvinyo!
2 [e]Tazama, Bwana anaye mmoja aliye
na uwezo na nguvu.
Kama dhoruba ya mvua ya mawe
na upepo uharibuo,
kama mvua inyeshayo kwa nguvu na
mafuriko yashukayo,
atakiangusha chini kwa nguvu.
3 [f]Lile taji la maua, kiburi cha walevi
cha Efraimu,
kitakanyagwa chini ya nyayo.
4 [g]Lile ua linalosinyaa, uzuri wa
utukufu wake,
uliowekwa kwenye kichwa cha
bonde lenye rutuba,
litakuwa kama tini iliyoiva kabla ya
mavuno:
mara mtu aionapo, huichuma na
kuila.

5 [h]Katika siku ile, BWANA Mwenye
Nguvu Zote
atakuwa taji la utukufu,
taji zuri la maua
kwa mabaki ya watu wake.
6 [i]Atakuwa roho ya haki
kwa yeye aketiye katika kiti cha
hukumu,
chanzo cha nguvu
kwa wale wazuiao vita langoni.

7 [j]Hawa pia wanapepesuka kwa
sababu ya mvinyo,
wanayumbayumba kwa sababu ya
kileo:
Makuhani na manabii wanapepesuka
kwa sababu ya kileo,
wanachanganyikiwa kwa sababu
ya mvinyo;
wanapepesuka wanapoona maono,
wanajikwaa wanapotoa maamuzi.
8 [k]Meza zote zimejawa na matapishi
wala hakuna sehemu hata ndogo
isiyokuwa na uchafu.

9 [l]"Yeye anajaribu kumfundisha nani?
Yeye anamwelezea nani ujumbe
wake?
Je, ni kwa watoto walioachishwa
kunyonya?
Je, ni wale ambao ndipo tu
wametolewa matitini?

---

[a]**27:11** Kum 32:18, 38; Yer 8:7; 4:22; Isa 9:17; 10:33; Yer 11:16; Isa 33:12; 41:8; 44:21-24
[b]**27:12** Mwa 15:18; Kum 30:4; Isa 1:9; Mt 3:12; Isa 21:10; 17:6
[c]**27:13** Hes 10:2; Amu 3:27; Mt 24:31; Isa 10:19; Hos 8:1; Law 25:9; Za 106:47
[d]**28:1** Isa 7:2; Law 10:9; Amo 6:6; Isa 10:5; 9:9; Hos 7:5; Isa 5:11; 8:7
[e]**28:2** Isa 30:30; 40:10; Yos 10:11; Eze 13:11; Isa 29:6; 8:7; Dan 9:26
[f]**28:3** Ay 40:12; Isa 5:5
[g]**28:4** Wim 2:13; Nah 3:12; Hos 9:10
[h]**28:5** Zek 9:16; Eze 21:26; Isa 10:20; 1:9; 29:18; Yer 13:18; Eze 16:12; Isa 62:3
[i]**28:6** Amu 9:44-45; 2Sam 14:20; 2Nya 32:8; Yn 5:30; Isa 11:2-4
[j]**28:7** Law 10:9; Isa 56:10-12; Efe 5:18; Za 107:27; Isa 24:2; 3:12; 22:13; 9:15
[k]**28:8** Yer 48:26
[l]**28:9** Yer 6:10; 1Pet 2:2; Za 32:8; Ebr 5:12-13; Yer 31:34; Isa 30:20; 48:17; 54:13

10 [a]Kwa maana ni:
Amri juu ya amri, amri juu ya amri,
kanuni juu ya kanuni, kanuni juu ya kanuni;
hapa kidogo, kule kidogo."

11 [b]Sawa kabisa, kwa midomo migeni
na kwa lugha ngeni,
Mungu atasema na watu hawa,
12 [c]wale ambao aliwaambia,
"Hapa ni mahali pa kupumzika,
waliochoka na wapumzike,"
na, "Hapa ni mahali pa mapumziko,"
lakini hawakutaka kusikiliza.
13 [d]Hivyo basi, neno la Bwana kwao litakuwa:
Amri juu ya amri, amri juu ya amri,
kanuni juu ya kanuni, kanuni juu ya kanuni,
hapa kidogo, kule kidogo:
ili waende na kuanguka chali,
wakijeruhiwa, wakinaswa na kukamatwa.

14 [e]Kwa hiyo sikieni neno la Bwana,
enyi watu wenye dharau
mnaotawala watu hawa wa Yerusalemu.
15 [f]Ninyi mnajisifu, "Tumefanya agano na mauti,
tumefanya mapatano na kuzimu.
Wakati pigo lifurikalo litakapopita,
haliwezi kutugusa sisi,
kwa kuwa tumefanya uongo kuwa kimbilio letu
na miungu ya uongo kuwa mahali petu pa kujificha."

16 [g]Kwa hiyo hivi ndivyo Bwana Mwenyezi asemavyo:

"Tazama, ninaweka jiwe katika Sayuni,
jiwe lililojaribiwa,
jiwe la pembeni la thamani kwa ajili ya msingi thabiti.
Yeye atumainiye kamwe hatatiwa hofu.
17 [h]Nitaifanya haki kuwa kamba ya kupimia
na uadilifu kuwa timazi;
mvua ya mawe itafagia kimbilio lenu, huo uongo,
nayo maji yatafurikia mahali penu pa kujificha.
18 [i]Agano lenu na kifo litabatilishwa,
patano lenu na kuzimu halitasimama.
Wakati pigo lifurikalo litakapowakumba,
litawaangusha chini.
19 [j]Kila mara lijapo litawachukua,
asubuhi baada ya asubuhi,
wakati wa mchana na wakati wa usiku,
litawakumba tangu mwanzo hadi mwisho."

Kuuelewa ujumbe huu
utaleta hofu tupu.
20 [k]Kitanda ni kifupi mno kujinyoosha juu yake,
nguo ya kujifunikia ni nyembamba mno
mtu hawezi kujifunikia.
21 [l]Bwana atainuka kama alivyofanya kwenye Mlima Perasimu,
ataghadhibika kama alivyofanya katika Bonde la Gibeoni:

[a]**28:10** Isa 29:13
[b]**28:11** Yer 5:15; 1Kor 14:21; Mwa 11:7; Eze 3:5; Isa 33:19
[c]**28:12** Yos 1:13; Mt 11:28-29; 2Nya 14:7; Kut 14:14; Ay 11:18; Isa 11:10
[d]**28:13** Mt 21:44; Isa 8:14-15
[e]**28:14** Isa 1:10; 2Nya 36:16
[f]**28:15** Dan 11:22; Isa 9:15; 10:26; Ay 5:23; Isa 8:19; Amu 9:35; Isa 29:15; Yer 23:24
[g]**28:16** Zek 12:3; Efe 2:20; Rum 9:33; 1Pet 2:6; Isa 54:4; 14:32; Za 118:22; Isa 8:14-15; Dan 2:34-45; Mdo 4:11; Yer 51:26; 1Kor 3:11
[h]**28:17** Isa 5:16; Za 11:7; 2Fal 21:13; Yos 10:11
[i]**28:18** Isa 63:18; Dan 8:13; Isa 7:7
[j]**28:19** 2Fal 24:2; Ay 18:11; Za 5:3
[k]**28:20** Isa 59:6
[l]**28:21** 2Sam 5:20; Mwa 38:29; 1Nya 14:11-16; Lk 19:41-44; Yos 9:3; Isa 65:7

ili kufanya kazi yake, kazi yake ya ajabu,
ili kutimiza kazi yake, kazi yake ngeni.
22 [a]Sasa acheni dharau zenu,
la sivyo minyororo yenu itakuwa mizito zaidi.
Bwana, BWANA Mwenye Nguvu Zote, ameniambia
habari za maangamizi yaliyoamriwa dhidi ya nchi yote.

23 [b]Sikilizeni msikie sauti yangu,
tegeni masikio na msikie niyasemayo.
24 [c]Wakati mkulima alimapo ili apande,
je, hulima siku zote?
Je, huendelea kubomoa ardhi
na kusawazisha udongo?
25 [d]Akiisha kusawazisha shamba,
je, hatapanyi mbegu za bizari na kutawanya jira?
Je, hapandi ngano katika sehemu yake,
shayiri katika eneo lake,
na nafaka nyingine katika shamba lake?
26 [e]Mungu wake humwelekeza
na kumfundisha njia iliyo sahihi.

27 [f]Iliki haipurwi kwa nyundo,
wala gurudumu la gari halivingirishwi juu ya jira;
iliki hupurwa kwa fimbo,
na jira kwa ufito.
28 [g]Nafaka lazima isagwe ili kutengeneza mkate,
kwa hiyo mtu haendelei kuipura daima.
Ingawa huendesha magurudumu ya gari lake la kupuria juu yake,
farasi wake hawasagi.

29 [h]Haya yote pia hutoka kwa BWANA Mwenye Nguvu Zote,
mwenye mashauri ya ajabu, na anayepita wote kwa hekima.

*Ole Wa Mji Wa Daudi*

29 [i]Ole wako, wewe Arieli, Arieli, mji alimokaa Daudi!
Ongezeni mwaka kwa mwaka,
na mzunguko wa sikukuu zenu uendelee.
2 [j]Hata hivyo nitauzunguka Arieli kwa jeshi,
utalia na kuomboleza,
utakuwa kwangu kama mahali
pa kuwashia moto madhabahuni.
3 [k]Nitapiga kambi pande zote dhidi yako,
nitakuzunguka kwa minara
na kupanga mazingirwa yangu dhidi yako.
4 [l]Utakaposhushwa, utanena kutoka ardhini,
utamumunya maneno yako kutoka mavumbini.
Sauti yako itatoka katika nchi kama vile ya mzimu,
utanong'ona maneno yako toka mavumbini.

5 [m]Lakini adui zako wengi watakuwa kama vumbi laini,
kundi la wakatili watakuwa
kama makapi yapeperushwayo.
Naam, ghafula, mara moja,
6 [n]BWANA Mwenye Nguvu Zote atakuja
na ngurumo, tetemeko la ardhi, na kwa sauti kuu,
atakuja na dhoruba, tufani na miali ya moto iteketezayo.

---

[a]**28:22** Isa 10:22; Yer 29:18; 2Nya 36:16; Mao 2:15; Sef 2:15
[b]**28:23** Isa 32:9
[c]**28:24** Mhu 3:2
[d]**28:25** Kut 9:32; Mt 23:23; Eze 4:9
[e]**28:26** Za 94:10
[f]**28:27** Isa 21:10; Ay 41:30; Isa 10:5
[g]**28:28** Isa 21:10
[h]**28:29** Yer 32:19; Za 92:5; Rum 11:33; Isa 9:5
[i]**29:1** Isa 22:12-13; 1:14; 2Sam 5:7; Isa 28:1
[j]**29:2** Mao 2:5; Isa 3:26; Eze 43:15
[k]**29:3** Lk 19:43-44; 2Fal 25:1
[l]**29:4** Isa 8:19; 47:1; 52:2; 26:16; Law 19:31
[m]**29:5** Isa 17:13; 1The 5:3; Za 55:15; Kum 9:21; Za 78:39; Isa 51:12; Za 103:15
[n]**29:6** Mk 13:8; Ufu 6:12; Isa 26:21; Zek 14:1-5; Kut 19:16; Mt 24:7; Za 83:13-15

[7] [a]Kisha makundi ya mataifa yote yale
yapiganayo dhidi ya Arieli,
yale yanayomshambulia yeye na
ngome zake, na kumzunguka
kwa jeshi,
watakuwa kama ilivyo ndoto,
kama maono wakati wa usiku:
[8] [b]kama vile mtu aliye na njaa aotavyo
kuwa anakula,
lakini huamka, bado njaa yake
ingalipo,
kama vile mtu mwenye kiu aotavyo
kuwa anakunywa maji,
lakini huamka akiwa anazimia,
akiwa bado angali ana kiu.
Hivyo ndivyo itakavyokuwa kwa
makundi yote ya mataifa
yanayopigana dhidi ya Mlima
Sayuni.

[9] [c]Duwaeni na kushangaa,
jifanyeni vipofu wenyewe na
msione,
leweni, lakini si kwa mvinyo,
pepesukeni lakini si kwa kileo.
[10] [d]BWANA amewaleteeni usingizi
mzito:
Amezibá macho yenu (ninyi
manabii);
amefunika vichwa vyenu (ninyi
waonaji).

[11] [e]Kwa maana kwenu ninyi, maono
haya yote si kitu ila maneno yaliyotiwa
lakiri katika kitabu. Kama mkimpa mtu
yeyote awezaye kusoma kitabu hiki,
nanyi mkamwambia, "Tafadhali kisome,"
yeye atajibu, "Mimi siwezi, kwa kuwa
kimetiwa lakiri." [12] Au kama mkimpa mtu
yeyote kitabu hiki asiyeweza kusoma na
kumwambia, "Tafadhali kisome," atajibu,
"Mimi sijui kusoma."

[13] [f]Bwana anasema:

"Watu hawa hunikaribia kwa vinywa
vyao
na kuniheshimu kwa midomo yao,
lakini mioyo yao iko mbali nami.
Ibada yao kwangu inatokana na
maagizo
waliyofundishwa na wanadamu.
[14] [g]Kwa hiyo mara nyingine tena
nitawashangaza watu hawa,
kwa ajabu juu ya ajabu.
Hekima ya wenye hekima itapotea,
nayo akili ya wenye akili
itatoweka."
[15] [h]Ole kwa wale wanaokwenda
kwenye vilindi virefu
kumficha BWANA mipango yao,
wafanyao kazi zao gizani na kufikiri,
"Ni nani anayetuona? Ni nani
atakayejua?"
[16] [i]Mnapindua mambo juu chini,
kana kwamba mfinyanzi aweza
kufikiriwa kuwa kama udongo
wa mfinyanzi!
Je, kile kilichofinyangwa
chaweza kumwambia yule
aliyekifinyanga,
"Wewe hukunifinyanga mimi?"
Je, chungu kinaweza kumwambia
mfinyanzi,
"Wewe hujui chochote?"

[17] [j]Kwa muda mfupi sana, je, Lebanoni
haitageuzwa kuwa shamba
lenye rutuba,
na shamba lenye rutuba liwe kama
msitu?

[a]**29:7** Mik 4:11-12; Zek 12:9; Ay 20:8
[b]**29:8** Za 73:20; Yer 30:16; Isa 17:12-14; Zek 12:3; Isa 54:17
[c]**29:9** Yer 13:13; Isa 63:9; Law 10:9; Yer 4:9; Isa 6:10; 63:6; Za 60:3; Yer 13:13; Isa 51:22
[d]**29:10** 2The 2:9-11; Za 69:23; Mik 3:6; Amu 4:21; Isa 44:18; 6:9-10; Rum 11:8
[e]**29:11** Dan 8:26; Mt 13:11; Isa 28:7; Ufu 5:1-2; Isa 8:16; Dan 12:9
[f]**29:13** Yer 12:2; Kol 2:22; Eze 33:31; Mt 15:8-9; Mk 7:6-7; Isa 58:2; Za 119:70; Yer 14:11
[g]**29:14** Yer 49:7; Ay 10:16; 5:13; Isa 6:9-10; 1Kor 1:19; Yer 8:9; Isa 6:9-10
[h]**29:15** Ay 22:13-14; Eze 8:12; 2Fal 21:16; Ay 22:13; Isa 28:15; Ay 8:3; Za 10:11-13
[i]**29:16** Yer 18:6; Rum 9:20-21; Za 94:9; Ay 10:9; Isa 10:15; 45:9; Ay 9:12; Yer 18:6; Mwa 2:7
[j]**29:17** Za 84:6; Isa 32:15; 10:25; 2:13; Za 107:33

18 [a]Katika siku ile viziwi watasikia
maneno ya kitabu,
na katika utusitusi na giza
macho ya kipofu yataona.
19 [b]Mara nyingine tena wanyenyekevu
watafurahi katika BWANA,
wahitaji watafurahi katika yeye
Aliye Mtakatifu wa Israeli.
20 [c]Wakatili watatoweka na wenye
kudhihaki watatokomea,
nao wote wenye jicho la uovu
watakatiliwa mbali,
21 [d]wale ambao kwa neno humfanya
mtu kuwa mwenye hatia,
wamtegeao mtego mtetezi katika
mahakama,
na kwa ushuhuda wa uongo
humnyima haki
yeye asiye na hatia.

22 [e]Kwa hiyo hili ndilo BWANA,
aliyemkomboa Abrahamu, analosema kwa
nyumba ya Yakobo:

"Yakobo hataaibishwa tena,
wala nyuso zao hazitabadilika sura
tena.
23 [f]Wakati watakapoona watoto wao
miongoni mwao,
kazi ya mikono yangu,
watalitakasa Jina langu takatifu;
wataukubali utakatifu wa yeye
Aliye Mtakatifu wa Yakobo,
nao watamcha Mungu wa Israeli.
24 [g]Wale wanaopotoka rohoni watapata
ufahamu,
nao wale wanaolalamika
watayakubali mafundisho."

*Ole Wa Taifa Kaidi*

30 [h]BWANA asema,
"Ole kwa watoto
wakaidi,
kwa wale wanaotimiza mipango
ambayo si yangu,
wakifanya makubaliano, lakini si
kwa Roho wangu,
wakilundika dhambi juu ya
dhambi,
2 [i]wale washukao kwenda Misri
bila kutaka shauri langu,
wanaotafuta msaada wa ulinzi wa
Farao,
watafutao kivuli cha Misri kwa
ajili ya kimbilio.
3 [j]Lakini ulinzi wa Farao utakuwa kwa
aibu yenu,
kivuli cha Misri kitawaletea
fedheha.
4 [k]Ingawa wana maafisa katika Soani
na wajumbe wamewasili katika
Hanesi,
5 [l]kila mmoja ataaibishwa
kwa sababu ya taifa lisilowafaa
kitu,
ambalo haliwaletei msaada wala
faida,
bali aibu tu na fedheha."

6 [m]Neno kuhusu wanyama wa Negebu:

Katika nchi ya taabu na shida,
ya simba za dume na jike,
ya nyoka mwenye sumu kali na
nyoka warukao,
wajumbe huchukua utajiri wao juu
ya migongo ya punda,
hazina zao juu ya nundu za
ngamia,

[a]**29:18** Mk 7:37; Za 146:8; Mt 11:5; Lk 7:22; Isa 32:3; Za 107:14
[b]**29:19** Za 72:4; 25:9; Isa 5:19; 12:6; 3:15; Yak 2:5; Mt 5:5; 11:29; Mwa 42:26
[c]**29:20** 2Nya 36:16; Isa 28:22; Eze 11:2; Isa 13:11; 59:4; Ay 15:35; Za 7:14
[d]**29:21** Amo 5:10-15; Isa 5:23; Hab 1:4; Mit 21:28
[e]**29:22** Mwa 11:16; Yoe 2:26; Yos 24:3; Sef 3:11; Kut 6:6; Mwa 17:16; Isa 41:8; 51:2
[f]**29:23** Isa 53:10; 54:1-4; 19:25; 49:20-26; 5:19; Mt 6:9
[g]**29:24** Mit 12:8; Ebr 5:2; Isa 60:16; 42:16; Za 95:10; Isa 28:7; 32:4
[h]**30:1** Isa 29:15; 8:12; Kum 29:19; 21:18; 2Fal 17:4
[i]**30:2** Mwa 25:22; Hes 27:21; 2Fal 25:26; Isa 36:6; Yer 2:18, 36; 42:14; Eze 17:15; 29:16
[j]**30:3** Yer 37:5-7; Isa 20:4-5; Amu 9:8-15; Za 44:13
[k]**30:4** Hes 13:22; Isa 19:11
[l]**30:5** Isa 20:5; 36:6; 2Fal 18:21; Za 108:12; Yer 37:3-5; Eze 17:15
[m]**30:6** Kut 1:3; Yer 11:4; Kum 8:15; Hos 8:9; Kut 5:10; Isa 13:1; 5:30; 5:29; Mwa 42:26

kwa lile taifa lisilokuwa na faida,
7 [a]kuvipeleka Misri,
ambaye msaada wake haufai kabisa.
Kwa hiyo nimemwita "Rahabu Asiyefanya Chochote."

8 [b]Nenda sasa, liandike neno hili juu ya kibao kwa ajili yao,
liandike kwenye kitabu,
ili liweze kuwa shahidi milele
kwa ajili ya siku zijazo.
9 [c]Hawa ni watu waasi, watoto wadanganyifu,
watoto ambao hawataki kusikiliza mafundisho ya BWANA.
10 [d]Wanawaambia waonaji,
"Msione maono tena!"
Nako kwa manabii wanasema,
"Msiendelee kutupatia maono
ambayo ni ya kweli!
Tuambieni mambo ya kupendeza,
tabirini mambo ya uongo.
11 [e]Acheni njia hii,
ondokeni katika mapito haya,
nanyi acheni kutukabili pamoja
na yeye Aliye Mtakatifu wa Israeli!"

12 [f]Kwa hiyo, hili ndilo asemalo yeye Aliye Mtakatifu wa Israeli:

"Kwa sababu mmekataa ujumbe huu,
mkategemea uonevu na kutumainia udanganyifu,
13 [g]dhambi hii itakuwa kwenu
kama ukuta mrefu,
wenye ufa na wenye kubetuka,
ambao unaanguka ghafula,
mara moja.
14 [h]Utavunjika vipande vipande kama chombo cha udongo
ukipasuka pasipo huruma
ambapo katika vipande vyake
hakuna kipande kitakachopatikana
kwa kuukulia makaa kutoka jikoni
au kuchotea maji kisimani."

15 [i]Hili ndilo BWANA Mwenyezi, yeye Aliye Mtakatifu wa Israeli, asemalo:

"Katika kutubu na kupumzika ndio wokovu wenu,
katika kutulia na kutumaini ndizo nguvu zenu,
lakini hamkutaka.
16 [j]Mlisema, 'Hapana, tutakimbia kwa farasi.'
Kwa hiyo mtakimbia!
Mlisema, 'Tutakimbia kwa farasi waendao kasi.'
Kwa hiyo wanaowafukuza watakwenda kasi!
17 [k]Watu 1,000 watakimbia
kwa ajili ya kitisho cha mtu mmoja,
kwa vitishio vya watu watano
wote mtakimbia,
hadi mtakapoachwa kama mlingoti wa bendera
juu ya kilele cha mlima,
kama bendera juu ya kilima."

18 [l]Hata hivyo BWANA anatamani kutupatia neema,
anainuka ili kuwaonyesha huruma.
Kwa kuwa BWANA ni Mungu wa haki.
Wamebarikiwa wote wanaomngojea yeye!

---

[a]**30:7** Yer 2:36; Ay 9:13; 2Fal 18:2
[b]**30:8** Kut 17:14; Hab 2:2; Kum 27:8; Yer 25:13; Yos 24:26-27; Isa 8:1; Yer 30:2
[c]**30:9** Isa 28:15; Kum 32:20; Isa 59:3-4; Za 78:8; Eze 2:6
[d]**30:10** Amo 7:13; Yer 11:21; 32:3; 1Sam 9:9; 1Fal 22:8; Yer 4:10; Eze 13:7; Rum 16:18; 2Tim 4:4
[e]**30:11** Mdo 13:8; Ay 21:14; Isa 35:8-9; Mit 3:6; Isa 29:19; 48:17
[f]**30:12** Isa 5:19; 5:24; Za 10:7; 12:5; Isa 5:7, 24
[g]**30:13** Neh 2:17; Za 80:12; 1Fal 20:30; Isa 17:14; Za 62:3
[h]**30:14** Za 2:9; 2Pet 2:4-5
[i]**30:15** Isa 32:17; 2Nya 20:12; Mt 23:37
[j]**30:16** Yer 46:6; Kum 17:16; 1Fal 10:28-29
[k]**30:17** Kum 28:25; 2Fal 7:7; Law 26:8; Yos 23:10
[l]**30:18** Mwa 43:31; 2Pet 3:9, 15; Za 27:14; Mao 3:25; Isa 5:16; 42:14; 48:9; Yon 3:10

19 [a]Enyi watu wa Sayuni, mnaoishi
Yerusalemu, hamtalia tena. Tazameni
jinsi atakavyokuwa na huruma mtakapolia
kwa kumwomba msaada! Mara asikiapo,
atawajibu. 20 [b]Ingawa Bwana huwapa
chakula cha shida na maji ya taabu, walimu
wenu hawatafichwa tena, kwa macho yenu
wenyewe mtawaona. 21 [c]Mkigeuka kuume
au kushoto, masikio yenu yatasikia sauti
nyuma yenu ikisema, “Hii ndiyo njia,
ifuateni.” 22 [d]Kisha mtanajisi sanamu zenu
zilizofunikwa kwa fedha, na vinyago vyenu
vilivyofunikwa kwa dhahabu. Mtazitupilia
mbali kama vitambaa vya wakati wa hedhi
na kuziambia, “Haya, tokeni hapa!”

23 [e]Pia atawapa mvua kwa ajili ya mbegu
mnazootesha ardhini, chakula kinachotoka
ardhini kitakuwa kizuri sana, tena tele.
Katika siku ile, ng’ombe wenu watalisha
katika shamba pana la majani. 24 [f]Maksai
na punda walimao watakula majani
makavu na vyakula vilivyotengenezwa,
vinavyotandazwa kwa uma na sepeto.
25 [g]Katika siku ile ya mauaji makuu,
wakati minara itakapoanguka, vijito vya
maji vitatiririka juu ya kila mlima mrefu
na kila kilima kilichoinuka sana. 26 [h]Mwezi
utaangaza kama jua, nao mwanga wa jua
utang’aa mara saba zaidi, kama nuru ya
siku saba, wakati BWANA atakapoyafunga
majeraha ya watu wake na kuwaponya
vidonda alivyowatia.

27 [i]Tazama, Jina la BWANA linakuja
kutoka mbali,
likiwa na hasira kali inayowaka
pamoja na wingu zito la moshi,
midomo yake imejaa ghadhabu
na ulimi wake ni moto ulao.
28 [j]Pumzi yake ni kama mkondo wa
maji yaendayo kasi,
yakipanda hadi shingoni.
Hutikisa mataifa katika chekecheke
ya uharibifu,
huweka lijamu katika mataya ya
mataifa
ambayo huwaongoza upotevuni.
29 [k]Nanyi mtaimba kama usiku ule
mnaadhimisha
sikukuu takatifu.
Mioyo yenu itashangilia
kama vile watu wanapokwea na
filimbi
kwenye mlima wa BWANA,
kwa Mwamba wa Israeli.
30 [l]BWANA atawasababisha watu
waisikie sauti yake ya
utukufu,
naye atawafanya wauone mkono
wake ukishuka
pamoja na hasira yake kali na moto
ulao,
kukiwa na tufani ya mvua,
ngurumo za radi na mvua ya
mawe.
31 [m]Sauti ya BWANA itaivunjavunja
Ashuru,
kwa fimbo yake ya utawala
atawapiga.
32 [n]Kila pigo BWANA atakaloliweka juu
yao
kwa fimbo yake ya kuadhibu,

[a]**30:19** Isa 61:3; Ay 22:27; Mt 7:7-11; Isa 25:8; Ay 24:12; Zek 13:9; Za 86:7; Isa 41:17
[b]**30:20** 1Fal 22:27; Za 74:9; Isa 28:9; Amo 8:11
[c]**30:21** Kum 5:32; Mit 4:27; Isa 29:24; Ay 33:11
[d]**30:22** Kut 32:4; Isa 2:20; Law 15:19-23; Eze 7:19-20
[e]**30:23** 1Tim 4:8; Za 65:13; Kum 28:12; Isa 65:21-22; Yer 31:14; Ay 36:31
[f]**30:24** Mt 3:12; Lk 3:17; Isa 32:14; Ay 6:5
[g]**30:25** Isa 13:5; Kut 17:6; Isa 32:2; Yoe 3:18
[h]**30:26** Zek 14:7-8; Ufu 21:23; 2Nya 7:14; Hos 14:4; Isa 60:19-20; Yer 3:22; 17:14
[i]**30:27** 1Fal 18:24; Isa 26:20; 60:14; Eze 22:31; Ay 41:21
[j]**30:28** 2The 2:8; Amo 9:9; 2Fal 19:28; Isa 37:29; 11:4; 28:15; Za 50:3
[k]**30:29** Mt 26:30; Za 42:4; Isa 25:9; 1Sam 10:5; Mwa 49:24
[l]**30:30** Kut 19:18; Za 29:3; Kut 20:18; Isa 47:14; 9:12
[m]**30:31** Isa 10:5, 12; 11:4
[n]**30:32** Isa 11:15; 10:26; Eze 32:10; Kut 15:20

litakuwa kwa wimbo wa matari na
vinubi,
anapopigana nao katika vita
kwa mapigo ya mkono wake.
33 [a]Tofethi imeandaliwa toka zamani,
imewekwa tayari kwa ajili ya
mfalme.
Shimo lake la moto limetengenezwa
kwa kina kirefu
na kwa upana mkubwa,
likiwa na moto na kuni tele;
pumzi ya BWANA,
kama kijito cha kiberiti,
huuwasha moto.

*Ole Wa Wale Wanaotegemea Misri*

31 [b]Ole wao wale washukao Misri
kwa ajili ya msaada,
wale wategemeao farasi,
wanaoweka tumaini katika wingi wa
magari yao ya vita,
na katika nguvu nyingi za
wapanda farasi,
lakini hawamwangalii yeye Aliye
Mtakatifu wa Israeli,
wala hawatafuti msaada kwa
BWANA.
2 [c]Hata hivyo yeye pia ana hekima na
anaweza kuleta maafa,
wala hayatangui maneno yake.
Yeye atainuka dhidi ya nyumba ya
mwovu,
dhidi ya wale ambao huwasaidia
watenda mabaya.
3 [d]Lakini Wamisri ni wanadamu, wala
si Mungu,
farasi wao ni nyama, wala si roho.
Wakati BWANA atakaponyoosha
Mkono wake,
yeye anayesaidia atajikwaa,
naye anayesaidiwa ataanguka,
wote wawili wataangamia pamoja.

4 [e]Hili ndilo BWANA analoniambia:

"Kama vile simba angurumavyo,
simba mkubwa juu ya mawindo
yake:
hata ingawa kundi lote la wachunga
mifugo
huitwa pamoja dhidi yake,
hatiwi hofu na kelele zao
wala kusumbuliwa na ghasia zao;
ndivyo BWANA Mwenye Nguvu Zote
atakavyoshuka
kufanya vita juu ya Mlima Sayuni
na juu ya vilele vyake.
5 [f]Kama ndege warukao,
BWANA Mwenye Nguvu Zote
ataukinga Yerusalemu;
ataukinga na kuuokoa,
atapita juu yake na kuufanya
salama."

6 [g]Mrudieni yeye ambaye nyumba ya
Israeli imemwasi sana. 7 [h]Kwa kuwa katika
siku ile kila mmoja wenu atazikataa sanamu
za fedha na za dhahabu zilizotengenezwa
kwa mikono yenu yenye dhambi.

8 [i]"Ashuru itaanguka kwa upanga
ambao si wa mwanadamu;
upanga usio wa kibinadamu
utawaangamiza.
Watakimbia mbele ya upanga
na vijana wao wa kiume
watafanyizwa kazi kwa
lazima.
9 [j]Ngome zao zitaanguka kwa sababu
ya hofu;
kwa kuona bendera ya vita,
majemadari wao watashikwa na
hofu ya ghafula,"

---

[a]**30:33** 2Fal 23:10; Yer 7:31; Mwa 19:24; Ufu 9:17; 2Sam 22:16
[b]**31:1** Eze 17:15; Kum 17:16; 20:1; Yer 37:5; Dan 9:13; Hos 11:8; Isa 30:2-5; Ay 6:10
[c]**31:2** Za 92:5; Rum 16:27; Hes 23:19; Mit 19:21; Isa 29:15; Amo 3:6; Isa 29:19; 32:6
[d]**31:3** Eze 28:9; Isa 20:5; Za 9:20; 2The 2:4; Ay 30:21; Yer 51:25; Isa 30:5-7; Neh 1:10
[e]**31:4** Nah 3:18; Ay 30:21; Isa 30:5-7; Hes 24:9; 1Sam 17:34; Eze 34:23; Isa 42:13; Hos 11:10
[f]**31:5** Za 91:4; Kum 32:11; Zek 9:15; Za 34:7; Mt 23:37; Kut 12:23
[g]**31:6** Ay 22:23; Isa 1:5, 27
[h]**31:7** Isa 2:20; 30:22; 1Fal 12:30; Za 135:5
[i]**31:8** Isa 10:12; Kut 12:12; Hab 2:8; Mwa 49:15; Isa 14:25; Yer 25:12; Kum 20:11
[j]**31:9** Kum 32:31-37; Isa 10:17; Law 6:13; Isa 18:3; Yer 4:6; 51:9; Za 21:9

asema BWANA,
ambaye moto wake uko Sayuni,
nayo tanuru yake iko Yerusalemu.

*Ufalme Wa Haki*

32 [a]Tazama, mfalme atatawala kwa uadilifu
na watawala watatawala kwa haki.
2 [b]Kila mtu atakuwa kama kivuli cha kujificha kutokana na upepo
na kimbilio kutokana na dhoruba,
kama vijito vya maji jangwani
na kivuli cha mwamba mkubwa katika ardhi yenye kiu.

3 [c]Ndipo macho ya wale wanaoona hayatafumbwa tena,
nayo masikio ya wale wanaosikia yatasikiliza.
4 [d]Moyo wa mtu mwenye hamaki utafahamu na kuelewa,
nao ulimi wenye kigugumizi utanena kwa ufasaha.
5 [e]Mpumbavu hataitwa tena muungwana,
wala mtu mbaya kabisa kupewa heshima ya juu.
6 [f]Kwa kuwa mpumbavu hunena upumbavu,
moyo wake hushughulika na uovu:
Hutenda mambo yasiyo ya kumcha Mungu,
na hueneza habari za makosa kuhusu BWANA;
yeye huwaacha wenye njaa bila kitu,
na wenye kiu huwanyima maji.
7 [g]Taratibu za mtu mbaya kabisa ni ovu,
hufanya mipango miovu
ili kumwangamiza maskini kwa uongo,
hata wakati ambapo hoja za mhitaji ni za haki.
8 [h]Lakini mtu muungwana hufanya mipango ya kiungwana,
na kwa matendo ya kiungwana yeye hufanikiwa.

*Wanawake Wa Yerusalemu*

9 [i]Enyi wanawake wenye kuridhika sana,
amkeni na mnisikilize.
Enyi binti mnaojisikia kuwa salama,
sikieni lile ninalotaka kuwaambia!
10 [j]Muda zaidi kidogo ya mwaka mmoja,
ninyi mnaojisikia salama mtatetemeka,
mavuno ya zabibu yatakoma
na mavuno ya matunda hayatakuwepo.
11 [k]Tetemekeni, enyi wanawake wenye kuridhika,
tetemekeni kwa hofu, enyi binti mnaojisikia salama!
Vueni nguo zenu,
vaeni nguo ya gunia viunoni mwenu.
12 [l]Pigeni matiti yenu kwa ajili ya mashamba mazuri,
kwa ajili ya mizabibu iliyozaa vizuri
13 [m]na kwa ajili ya nchi ya watu wangu,
nchi ambayo miiba na michongoma imemea:
naam, ombolezeni kwa ajili ya nyumba zote za furaha
na kwa ajili ya mji huu wenye kufanya sherehe.

[a]**32:1** 2Nya 31:20; Eze 37:24; Za 72:1-4; Yer 23:5; Isa 28:6; Za 149:2; Isa 6:5
[b]**32:2** 1Fal 18:4; Isa 4:6; Za 55:8; 23:2; Isa 49:10; Yer 31:9; Za 107:35
[c]**32:3** Isa 29:18; 42:7, 16; Kum 29:4
[d]**32:4** Isa 6:10; 29:24; 35:6
[e]**32:5** 1Sam 25:25
[f]**32:6** Isa 3:15; Mit 19:3; Isa 9:16-17; Mit 24:2; Isa 26:10
[g]**32:7** Yer 5:26-28; Dan 12:10; Mik 7:3; Isa 29:19-20; Za 72:4; Isa 29:21
[h]**32:8** 1Nya 29:9; Mit 11:25; Isa 14:24
[i]**32:9** Isa 28:23; Dan 4:4; Amo 6:1; Sef 2:15
[j]**32:10** Isa 5:5-6; 24:7; 37:30
[k]**32:11** Nah 3:5; Mik 1:8; Isa 34:14; 47:2; 3:24
[l]**32:12** Nah 2:7; Isa 16:9
[m]**32:13** Hos 9:6; 10:8; Isa 23:7; 24:11

14 [a]Ngome itaachwa,
mji wenye kelele nyingi
utahamwa,
ngome ndani ya mji na mnara wa
ulinzi vitakuwa ukiwa milele,
mahali pazuri pa punda na
malisho ya makundi ya
kondoo,
15 [b]mpaka Roho amwagwe juu yetu
kutoka juu,
nalo jangwa kuwa shamba lenye
rutuba,
na shamba lenye rutuba kuwa
kama msitu.
16 [c]Haki itakaa katika jangwa,
na uadilifu utakaa katika shamba
lenye rutuba.
17 [d]Matunda ya haki yatakuwa amani,
matokeo ya haki yatakuwa utulivu
na matumaini milele.
18 [e]Watu wangu wataishi katika makao
ya mahali pa amani,
katika nyumba zilizo salama,
katika mahali pa kupumzika
pasipo na usumbufu.
19 [f]Hata kama mvua ya mawe iangushe
msitu
na mji ubomolewe kabisa,
20 [g]tazama jinsi utakavyobarikiwa,
ukipanda mbegu yako katika kila
kijito,
na kuwaacha ng'ombe wako
na punda wajilishe kwa uhuru.

[a]**32:14** Isa 13:22; 27:10; 2:15; 34:13; 6:11; 5:17; Za 104:11
[b]**32:15** Yoe 2:28; Eze 37:9; Za 107:35; Isa 29:17; 11:2
[c]**32:16** Isa 9:7; 28:6; 35:1, 6; 42:11; Za 48:1; Isa 1:26
[d]**32:17** Za 85:10; 119:165; Rum 14:17; Ebr 12:11
[e]**32:18** Yos 1:13; 11:18; Hos 2:18-23; Amo 9:14
[f]**32:19** Isa 19:18; 24:10; 28:17; 30:30; Zek 11:2; Ay 40:11
[g]**32:20** Mhu 11:1; Isa 30:24; Ay 39:8; Kum 28:12

*Taabu Na Msaada*

33 [h]Ole wako wewe, ee mharabu,
wewe ambaye
hukuharibiwa!
Ole wako, ee msaliti,
wewe ambaye hukusalitiwa!
Utakapokwisha kuharibu,
utaharibiwa;
utakapokwisha kusaliti,
utasalitiwa.

2 [i]Ee BWANA, uturehemu,
tunakutamani.
Uwe nguvu yetu kila asubuhi
na wokovu wetu wakati wa taabu.
3 [j]Kwa ngurumo ya sauti yako, mataifa
yanakimbia;
unapoinuka, mataifa hutawanyika.
4 [k]Mateka yenu, enyi mataifa,
yamevunwa kama vile
wafanyavyo madumadu,
kama kundi la nzige watu
huvamia juu yake.

5 [l]BWANA ametukuka, kwa kuwa
anakaa mahali palipoinuka,
ataijaza Sayuni kwa haki na
uadilifu.
6 [m]Atakuwa msingi ulio imara kwa
wakati wenu,
ghala za wokovu tele, hekima na
maarifa;
kumcha BWANA ni ufunguo wa
hazina hii.

7 [n]Angalia, watu wake mashujaa
wanapiga kelele kwa nguvu
barabarani,
wajumbe wa amani wanalia kwa
uchungu.

[h]**33:1** Hab 2:8; Yer 30:16; Eze 39:10; 2Fal 19:21; Isa 31:8; 21:2; Mt 7:2
[i]**33:2** Za 13:5; Isa 59:16; 25:9; 5:30; Ezr 9:8; Mwa 43:29; Isa 40:10
[j]**33:3** Za 12:5; Hes 10:35; Za 46:6; 68:33; Isa 59:16-18
[k]**33:4** Hes 14:3; 2Fal 7:16; Isa 17:5; Yoe 3:13
[l]**33:5** Za 97:9; Isa 5:16; 28:6; Ay 16:19; Isa 9:7; 1:26
[m]**33:6** Isa 12:2; Mt 6:33; Mit 1:7; Mwa 39:3; Ay 22:25; 1Sam 11:2-3
[n]**33:7** Isa 10:34; 2Fal 18:37

8 [a]Njia kuu zimeachwa,
hakuna wasafiri barabarani.
Mkataba umevunjika,
mashahidi wake
wamedharauliwa,[b]
hakuna yeyote anayeheshimiwa.
9 [c]Ardhi inaomboleza[d] na kuchakaa,
Lebanoni imeaibika na kunyauka,
Sharoni ni kama Araba,
nayo Bashani na Karmeli
wanapukutisha majani yao.

10 [e]"Sasa nitainuka," asema BWANA.
"Sasa nitatukuzwa;
sasa nitainuliwa juu.
11 [f]Mlichukua mimba ya makapi,
mkazaa mabua,
pumzi yenu ni moto uwateketezao.
12 [g]Mataifa yatachomwa kama
ichomwavyo chokaa,
kama vichaka vya miiba
vilivyokatwa ndivyo
watakavyochomwa."

13 [h]Ninyi mlio mbali sana, sikieni lile
nililofanya;
ninyi mlio karibu, tambueni
uweza wangu!
14 [i]Wenye dhambi katika Sayuni
wametiwa hofu,
kutetemeka kumewakumba
wasiomcha Mungu:
"Ni nani miongoni mwetu awezaye
kuishi na moto ulao?
Ni nani miongoni mwetu awezaye
kuishi na moto unaowaka
milele?"

15 [j]Yeye aendaye kwa uadilifu
na kusema lililo haki,
yeye anayekataa faida ipatikanayo
kwa dhuluma
na kuizuia mikono yake isipokee
rushwa,
yeye azuiaye masikio yake dhidi ya
mashauri ya mauaji,
na yeye afumbaye macho yake
yasitazame sana uovu:
16 [k]huyu ndiye mtu atakayeishi mahali
pa juu,
ambaye kimbilio lake litakuwa
ngome ya mlimani.
Atapewa mkate wake,
na maji yake hayatakoma.

17 [l]Macho yenu yatamwona mfalme
katika uzuri wake
na kuiona nchi inayoenea mbali.
18 [m]Katika mawazo yenu mtaifikiria
hofu iliyopita:
"Yuko wapi yule afisa mkuu?
Yuko wapi yule aliyechukua
ushuru?
Yuko wapi afisa msimamizi wa
minara?"
19 [n]Hutawaona tena wale watu wenye
kiburi,
wale watu wenye usemi wa
mafumbo,
wenye lugha ngeni, isiyoeleweka.

20 [o]Mtazame Sayuni, mji wa sikukuu
zetu;
macho yenu yatauona Yerusalemu,
mahali pa amani pa kuishi, hema
ambalo halitaondolewa,
nguzo zake hazitang'olewa kamwe,
wala hakuna kamba yake yoyote
itakayokatika.

---

[a]**33:8** Amu 5:6; Isa 30:21; 60:15; Zek 7:14; 2Fal 18:14
[b]8 Au: miji yake imedharauliwa.
[c]**33:9** Isa 3:26; 2Fal 19:23; Isa 24:4; 3:26; Yer 22:6; Kum 32:35-43; Mik 7:14
[d]9 Au: Ardhi inakauka.
[e]**33:10** Isa 33:3; 2:21; 5:16
[f]**33:11** Za 7:14; Yak 1:5; Isa 26:18; 59:4
[g]**33:12** Amo 2:1; Isa 5:6; 10:17; 27:11
[h]**33:13** Za 48:10; Isa 48:16; 49:1
[i]**33:14** Isa 32:11; Zek 13:9; Ebr 12:29; Isa 30:30; 1:28-31
[j]**33:15** Za 15:2; 119:37; Isa 58:8; Za 24:4; Eze 22:13; Mit 15:27
[k]**33:16** Isa 25:4; Za 18:1-2; Isa 65:13; Kum 32:13; Isa 48:21; 49:10
[l]**33:17** Isa 6:5; 4:2; 26:10
[m]**33:18** 1Kor 1:20; Isa 17:14; 2:15
[n]**33:19** Mwa 11:7; Yer 5:15; Isa 28:11
[o]**33:20** Isa 32:18; Za 46:5; 125:1-2; Mwa 26:22; Isa 41:18; 48:18

21 [a]Huko BWANA atakuwa Mwenye
Nguvu wetu.
Patakuwa kama mahali pa mito
mipana na vijito.
Hakuna jahazi lenye makasia
litakalopita huko,
wala hakuna meli yenye nguvu
itakayopita huko.
22 [b]Kwa kuwa BWANA ni mwamuzi
wetu,
BWANA ndiye mtoa sheria wetu,
BWANA ni mfalme wetu,
yeye ndiye atakayetuokoa.

23 [c]Kamba zenu za merikebu zimelegea:
Mlingoti haukusimama imara,
nalo tanga halikukunjuliwa.
Wingi wa mateka yatagawanywa,
hata yeye aliye mlemavu
atachukua nyara.
24 [d]Hakuna yeyote aishiye Sayuni
atakayesema, "Mimi ni
mgonjwa";
nazo dhambi za wale waishio
humo zitasamehewa.

*Hukumu Dhidi Ya Mataifa*

34 [e]Njooni karibu, enyi mataifa,
nanyi msikilize;
sikilizeni kwa makini,
enyi kabila za watu!
Dunia na isikie, navyo vyote vilivyo
ndani yake,
ulimwengu na vyote vitokavyo
ndani yake!
2 [f]BWANA ameyakasirikia mataifa
yote;
ghadhabu yake ni juu ya majeshi
yao yote.
Atawaangamiza kabisa,
atawatia mikononi mwa
wachinjaji.
3 [g]Waliouawa watatupwa nje,
maiti zao zitatoa uvundo,
milima itatota kwa damu zao.
4 [h]Nyota zote za mbinguni zitayeyuka
na anga litasokotwa kama kitabu,
jeshi lote la angani litaanguka
kama majani yaliyonyauka kutoka
kwenye mzabibu,
kama tini iliyonyauka kutoka
kwenye mtini.

5 [i]Upanga wangu umekunywa na
kushiba huko mbinguni,
tazama, unashuka katika hukumu
juu ya Edomu,
wale watu ambao
nimeshawahukumu,
kuwaangamiza kabisa.
6 [j]Upanga wa BWANA umeoga katika
damu,
umefunikwa na mafuta ya nyama:
damu ya kondoo na mbuzi,
mafuta kutoka figo za kondoo
dume.
Kwa maana BWANA ana dhabihu
huko Bosra,
na machinjo makuu huko Edomu.
7 [k]Nyati wataanguka pamoja nao,
ndama waume na mafahali
wakubwa.
Nchi yao italowana kwa damu,
nayo mavumbi yataloa mafuta ya
nyama.

---

[a]**33:21** Kut 17:6; Nah 3:8; Zek 2:5; Isa 10:34
[b]**33:22** Yak 4:12; Mt 21:5; Isa 11:4; Za 89:18; Isa 2:3
[c]**33:23** 2Fal 7:8-16
[d]**33:24** Hes 23:21; Rum 11:27; 1Yn 1:7-9; Isa 30:26; 2Nya 6:21; Yer 31:34; 33:18
[e]**34:1** Isa 43:9; Kum 4:26; 32:1; Za 24:1; Isa 33:13
[f]**34:2** Isa 13:5; Zek 5:3; Isa 10:25; 30:25
[g]**34:3** Yoe 2:20; Amo 4:10; Eze 38:22; Isa 5:25; Za 110:6; Eze 5:17; 14:19
[h]**34:4** 2Pet 3:10; Yoe 2:31; Eze 32:7-8; Ay 9:7; Ufu 6:13; Isa 13:13; Mt 24:29; Ay 8:12; Mk 13:15; Isa 15:6; Ebr 1:12
[i]**34:5** Yer 49:7; 46:10; Zek 13:7; 2Sam 8:13-14; Yos 6:17; Kum 32:41-42; Amo 3:14-15; Yer 47:6; Eze 21:5; 2Nya 28:17; Amo 1:11-12; 6:11; Mal 1:4
[j]**34:6** Kum 32:41; Law 3:9; Mwa 36:33; Isa 30:25; Yer 25:34; Ufu 19:17
[k]**34:7** Hes 23:22; Za 68:30; 2Sam 1:22

[8] [a]Kwa sababu BWANA anayo siku ya
kulipiza kisasi,
mwaka wa malipo,
siku ya kushindania shauri la
Sayuni.
[9] [b]Vijito vya Edomu vitageuka kuwa
lami,
mavumbi yake yatakuwa kiberiti
kiunguzacho,
nchi yake itakuwa lami iwakayo!
[10] [c]Haitazimishwa usiku wala mchana,
moshi wake utapaa juu milele.
Kutoka kizazi hadi kizazi itakuwa
ukiwa,
hakuna mtu yeyote atakayepita
huko tena.
[11] [d]Bundi wa jangwani na bundi
mwenye sauti nyembamba
wataimiliki,
bundi wakubwa na kunguru
wataweka viota humo.
Mungu atanyoosha juu ya Edomu
kamba ya kupimia ya machafuko
matupu,
na timazi ya ukiwa.
[12] [e]Watu wake wa kuheshimiwa
hawatakuwa na chochote
kitakachoitwa ufalme huko,
nao wakuu wao wote watatoweka.
[13] [f]Miiba itaenea katika ngome za
ndani,
viwawi na michongoma itaota
kwenye ngome zake.
Itakuwa maskani ya mbweha,
makao ya bundi.
[14] [g]Viumbe vya jangwani vitakutana na
fisi,
nao mbuzi-mwitu watalia
wakiitana;
huko viumbe vya usiku vitastarehe
pia
na kujitafutia mahali pa
kupumzika.
[15] [h]Bundi wataweka viota huko na
kutaga mayai,
atayaangua na kutunza makinda
yake
chini ya uvuli wa mabawa yake;
pia huko vipanga watakusanyika,
kila mmoja na mwenzi wake.

[16] [i]Angalieni katika gombo la BWANA na
msome:

Hakuna hata mmoja katika hawa
atakayekosekana,
hakuna hata mmoja atakayemkosa
mwenzi wake.
Kwa kuwa ni kinywa chake Mungu
kimeagiza,
na Roho wake atawakusanya
pamoja.
[17] [j]Huwagawia sehemu zao,
mkono wake huwagawanyia kwa
kipimo.
Wataimiliki hata milele
na kuishi humo kutoka kizazi hadi
kizazi.

*Furaha Ya Waliokombolewa*

35 [k]Jangwa na nchi kame vitafurahi;
nyika itashangilia na
kuchanua maua.
Kama waridi, [2] [l]litachanua maua,
litashangilia sana na kupaza sauti
kwa furaha.
Litapewa utukufu wa Lebanoni,
fahari ya Karmeli na Sharoni;
wataona utukufu wa BWANA,
fahari ya Mungu wetu.

[a]**34:8** Isa 2:12; 1:24; 59:18; Yoe 3:4; Eze 25:12-17; Amo 1:6-10
[b]**34:9** Mwa 19:24
[c]**34:10** Ufu 14:10-11; 19:3; Yer 49:18; Mal 1:3; Isa 13:20; Eze 29:12; 35:3
[d]**34:11** Law 11:16-18; Ufu 18:2; Mao 2:8; Amo 7:8; Kum 14:15-17; Yoe 3:19; 2Fal 21:13
[e]**34:12** Isa 41:11-12; Za 107:10; Ay 12:21; Isa 40:23; Eze 24:5; Yer 39:6
[f]**34:13** Hos 9:6; Isa 32:13; 13:22; Yer 9:11; Isa 7:19; Za 44:19
[g]**34:14** Za 74:14; Isa 13:22; Ufu 18:2
[h]**34:15** Za 17:8; Kum 14:13
[i]**34:16** Isa 30:8; Dan 7:10; Isa 1:20; 58:14; 48:13
[j]**34:17** Za 78:55; Isa 17:14; Yer 13:25
[k]**35:1** Isa 27:10; 41:18-19; 51:3; 32:15-16; 27:6
[l]**35:2** Wim 7:5; Mwa 21:6; Ezr 3:7; Za 105:43; Isa 32:15; 12:6; 25:9; 1Nya 27:29

3 [a]Itieni nguvu mikono iliyo dhaifu,
yafanyeni imara magoti
yaliyolegea,
4 [b]waambieni wale wenye mioyo ya
hofu,
"Kuweni hodari, msiogope;
tazama, Mungu wenu atakuja,
pamoja na malipo ya Mungu,
atakuja na kuwaokoa ninyi."

5 [c]Ndipo macho ya vipofu
yatafumbuliwa
na masikio ya viziwi yatazibuliwa.
6 [d]Ndipo kilema atarukaruka kama
kulungu,
nao ulimi wa aliye bubu utapaza
sauti kwa shangwe.
Maji yatatiririka kwa kasi katika
nyika,
na vijito katika jangwa.
7 [e]Mchanga wa moto utakuwa bwawa
la maji,
ardhi yenye kiu itabubujika
chemchemi.
Maskani ya mbweha walikolala hapo
awali
patamea majani, matete na
mafunjo.

8 [f]Nako kutakuwa na njia kuu,
nayo itaitwa Njia ya Utakatifu.
Wasio safi hawatapita juu yake;
itakuwa ya wale watembeao
katika Njia ile;
yeye asafiriye juu yake,
ajapokuwa mjinga, hatapotea.
9 [g]Huko hakutakuwepo na simba,
wala mnyama mkali hatapita njia
hiyo,
wala hawatapatikana humo.
Ila waliokombolewa tu ndio
watakaopita huko,
10 [h]waliokombolewa na BWANA
watarudi.
Wataingia Sayuni wakiimba;
furaha ya milele itakuwa juu ya
vichwa vyao.
Watapata furaha na shangwe;
huzuni na majonzi vitakimbia.

*Senakeribu Atishia Yerusalemu*

**(2 Wafalme 18:13-27; 2 Nyakati 32:1-19)**

36 [i]Katika mwaka wa kumi na nne
wa utawala wa Mfalme Hezekia,
Senakeribu mfalme wa Ashuru
akaishambulia miji yote ya Yuda yenye
ngome na kuiteka.
2 [j]Kisha mfalme wa
Ashuru akamtuma jemadari wa jeshi
pamoja na jeshi kubwa kutoka Lakishi hadi
kwa Mfalme Hezekia huko Yerusalemu.
Jemadari wa jeshi akasimama kwenye
mfereji wa Bwawa la Juu, lililojengwa
katika barabara iendayo kwenye Uwanja
wa Dobi.
3 [k]Eliakimu mwana wa Hilkia
aliyekuwa msimamizi wa jumba la kifalme,
Shebna aliyekuwa katibu, na Yoa mwana
wa Asafu mwandishi wakamwendea.
4 Jemadari wa jeshi akawaambia,
"Mwambieni Hezekia,

" 'Hili ndilo asemalo mfalme mkuu,
mfalme wa Ashuru: Ni wapi unapoweka
hili tumaini lako?
5 [l]Unasema mnayo
mikakati na nguvu za kijeshi, lakini
unasema maneno matupu tu. Je, wewe
unamtegemea nani, hata ukaniasi

[a]**35:3** Ay 4:3-4; Ebr 12:12
[b]**35:4** Isa 40:2; 2Nya 32:6; Zek 1:13; Kum 20:3; Isa 21:4; Yos 1:9; Isa 7:4; 1:24; 34:8; 25:9; 40:1; 10:9, 10-11; 51:5; 62:11; Dan 10:19; Ufu 22:12
[c]**35:5** Mt 9:27; 11:5; Isa 42:18; 29:18; 2Nya 32:6; Isa 40:2; Zek 1:13; Isa 21:4; Ufu 22:12
[d]**35:6** Lk 7:22; Yn 5:8-9; Mk 7:35; Kut 17:6; Yn 7:38; Mdo 3:2; Mt 15:30; Mdo 3:8
[e]**35:7** Za 68:6; Isa 41:17; 44:3; 55:1; 49:10; 58:11; 13:22; Za 107:35; Ay 8:11; 40:21
[f]**35:8** Yer 31:21; Yoe 3:17; Mt 7:13-14; 1Pet 1:15; Isa 52:1; 33:8
[g]**35:9** Isa 30:9; 11:6-9; Law 25:47-55; Kut 6:6; Isa 13:22; 62:12
[h]**35:10** Yn 16:22; Isa 51:11; 30:29; Ufu 21:4; Ay 19:25; Za 51:8
[i]**36:1** 2Nya 32:1; 2Fal 18:9; Za 109:11
[j]**36:2** Isa 7:3; Yos 10:3
[k]**36:3** 2Fal 18:18; Isa 37:2; 22:20-21; Mik 1:13; 2Sam 8:17; Mwa 41:40; 2Sam 8:16
[l]**36:5** 2Fal 18:7

mimi? [6] [a]Tazama sasa, unaitegemea
Misri, fimbo ile ya mwanzi uliopasuka,
ambayo huuchoma na kuujeruhi
mkono wa mtu akiiegemea! Hivyo
ndivyo alivyo Farao mfalme wa Misri,
kwa wote wanaomtegemea. [7] [b]Nawe
kama ukiniambia, "Tunamtumainia
BWANA Mungu wetu": je, siyo yeye
ambaye Hezekia aliondoa mahali
pake pa juu pa kuabudia miungu na
madhabahu zake, akiwaambia Yuda
na Yerusalemu, "Ni lazima mwabudu
mbele ya madhabahu haya"?
[8] [c]" 'Njooni sasa, fanyeni mapatano
na bwana wangu, mfalme wa Ashuru:
Nitakupa farasi elfu mbili, kama
unaweza kuwapandisha waendesha
farasi juu yao! [9] [d]Utawezaje kumzuia
hata afisa mmoja aliye mdogo kati
ya maafisa wa bwana wangu, ijapo
unategemea Misri kwa magari ya
vita na wapanda farasi? [10] [e]Zaidi ya
hayo, je, nimekuja kushambulia na
kuangamiza nchi hii bila BWANA?
BWANA mwenyewe ndiye aliniambia
niishambulie nchi hii na kuiangamiza.' "

[11] [f]Ndipo Eliakimu, Shebna na Yoa
wakamwambia yule jemadari wa jeshi,
"Tafadhali zungumza na watumishi
wako kwa lugha ya Kiaramu, kwa kuwa
tunaifahamu. Usiseme nasi kwa Kiebrania
watu walioko juu ya ukuta wakiwa
wanasikia."
[12] [g]Lakini yule jemadari wa jeshi akajibu,
"Je, bwana wangu amenituma kutoa
ujumbe huu kwa bwana wenu na kwenu
tu? Je, hakunituma pia kwa watu walioketi
ukutani, ambao, kama ninyi, itawabidi kula
mavi yao na kunywa mikojo yao wenyewe?"
[13] [h]Kisha yule jemadari wa jeshi
akasimama na kuita kwa lugha ya Kiebrania,
akasema: "Sikieni maneno ya mfalme mkuu,
mfalme wa Ashuru! [14] [i]Hili ndilo asemalo
mfalme: Msikubali Hezekia awadanganye.
Hawezi kuwaokoa! [15] [j]Msikubali Hezekia
awashawishi kumtumaini BWANA kwa
kuwaambia, 'Hakika BWANA atatuokoa. Mji
huu hautaangukia mikononi mwa mfalme
wa Ashuru.'
[16] [k]"Msimsikilize Hezekia. Hili ndilo
mfalme wa Ashuru asemalo: Fanyeni amani
nami na mje kwangu. Kisha kila mmoja
wenu atakula kutoka kwa mzabibu wake
na mtini wake mwenyewe, na kunywa maji
kutoka kisima chake mwenyewe, [17] [l]mpaka
nije nikawapeleke katika nchi iliyo kama
nchi yenu wenyewe, nchi ya nafaka na divai
mpya, nchi ya mkate na ya mashamba ya
mizabibu.
[18] "Msikubali Hezekia awapotoshe
asemapo, 'BWANA atatuokoa.' Je, yuko
mungu wa taifa lolote aliyewahi kuokoa
nchi yake kutoka mkononi mwa mfalme wa
Ashuru? [19] [m]Iko wapi miungu ya Hamathi na
ya Arpadi? Iko wapi miungu ya Sefarvaimu?
Je, imeokoa Samaria kutoka mkononi
mwangu? [20] [n]Ni yupi miongoni mwa miungu
yote ya nchi hizi ameweza kuokoa nchi
yake mkononi mwangu? Inawezekanaje
basi BWANA aiokoe Yerusalemu mkononi
mwangu?"
[21] [o]Lakini wale watu wakakaa kimya,
wala hawakujibu lolote, kwa kuwa mfalme
alikuwa amewaamuru, "Msimjibu lolote."
[22] [p]Kisha Eliakimu mwana wa Hilkia
msimamizi wa jumba la kifalme, Shebna
katibu, na Yoa mwana wa Asafu, mwandishi
wakamwendea Hezekia, nguo zao zikiwa

[a]**36:6** Isa 30:2-5; 58:5; Eze 29:6-7; 2Fal 17:4; Isa 8:12; Eze 17:17
[b]**36:7** Kum 12:2-5; 2Fal 18:4; 2Nya 31:1; Za 22:8; Mt 27:43
[c]**36:8** Za 20:7; Isa 30:16
[d]**36:9** Za 20:7; Isa 30:2-5; 31:3
[e]**36:10** 1Fal 13:18; Isa 10:5-7
[f]**36:11** Ezr 4:7
[g]**36:12** 2Fal 6:25; Eze 4:12
[h]**36:13** 2Nya 32:18; Isa 37:4
[i]**36:14** 2Nya 32:15
[j]**36:15** Isa 37:10; Za 3:2-7
[k]**36:16** 1Fal 4:25; Zek 3:10; Mik 4:4; Mit 5:15
[l]**36:17** 2Fal 15:29; Mwa 27:28; Kum 28:51
[m]**36:19** Hes 34:8; Yos 13:5; 2Fal 18:34; 17:24; 15:29
[n]**36:20** 1Fal 20:23; Dan 3:15; 2Nya 32:15; 25:15; Kut 5:2; Isa 10:8-11
[o]**36:21** Amo 5:13; Mit 9:7-8; 26:4
[p]**36:22** Mwa 37:29; 1Sam 4:12; Ay 1:20; 2Fal 18:18; 2Sam 8:16; 2Nya 34:19

zimeraruliwa, na kumwambia yale jemadari
wa jeshi aliyoyasema.

*Kuokolewa Kwa Yerusalemu Kunatabiriwa*

**(2 Wafalme 19:1-7)**

37 [a]Mfalme Hezekia aliposikia haya,
akararua nguo zake na kuvaa nguo
ya gunia, naye akaenda katika Hekalu
la Bwana. 2 [b]Akawatuma Eliakimu
msimamizi wa nyumba ya mfalme, Shebna
mwandishi, na viongozi wa makuhani,
wote wakiwa wamevaa nguo za magunia,
waende kwa nabii Isaya mwana wa Amozi.
3 [c]Wakamwambia, "Hili ndilo asemalo
Hezekia: Siku hii ni siku ya dhiki, ya
kukaripiwa na ya aibu, kama wakati watoto
wanapofikia karibu kuzaliwa na kumbe
hakuna nguvu ya kuwazaa. 4 [d]Yamkini
Bwana, Mungu wako atayasikia maneno
ya jemadari wa jeshi, ambaye bwana wake,
mfalme wa Ashuru, amemtuma kumdhihaki
Mungu aliye hai, tena kwamba atamkemea
kwa maneno ambayo Bwana, Mungu wako
ameyasikia. Kwa hiyo omba kwa ajili ya
mabaki ambao bado wako."

5 Maafisa wa Mfalme Hezekia walipofika
kwa Isaya, 6 [e]Isaya akawaambia, "Mwambieni
bwana wenu, 'Hili ndilo asemalo Bwana:
Usiogope kwa hayo uliyoyasikia, yale
maneno ambayo watumishi wa mfalme
wa Ashuru wamenitukana nayo. 7 [f]Sikiliza!
Nitatia roho fulani ndani yake ili kwamba
atakaposikia taarifa fulani, atarudi nchi
yake mwenyewe, nami huko nitafanya
auawe kwa upanga.' "

8 [g]Jemadari wa jeshi aliposikia kwamba
mfalme wa Ashuru ameondoka Lakishi,
alirudi, akamkuta mfalme akipigana na
Libna.

9 [h]Basi Senakeribu akapata taarifa
kwamba Tirhaka, Mkushi mfalme wa Misri,
alikuwa anaenda kupigana naye. Aliposikia
jambo hili akatuma wajumbe kwa Hezekia
na neno hili: 10 [i]"Mwambieni Hezekia
mfalme wa Yuda: Usikubali huyo Mungu
unayemtumainia akudanganye wakati
anaposema, 'Yerusalemu haitatiwa mkononi
mwa mfalme wa Ashuru.' 11 [j]Hakika
umesikia yale ambayo wafalme wa Ashuru
wametenda kwa nchi zote, wakiwaangamiza
kabisa. Je, wewe utaokolewa? 12 [k]Je, miungu
ya mataifa ambayo yaliangamizwa na baba
zangu iliweza kuwaokoa? Yaani miungu
ya Gozani, Harani, Resefu, na ya watu wa
Edeni waliokuwa Telasari? 13 [l]Yuko wapi
mfalme wa Hamathi, mfalme wa Arpadi,
mfalme wa mji wa Sefarvaimu, au wa Hena
au wa Iva?"

*Maombi Ya Hezekia*

14 [m]Hezekia akapokea barua kutoka kwa
wale wajumbe naye akaisoma. Kisha
akapanda katika Hekalu la Bwana,
akaikunjua mbele za Bwana. 15 [n]Naye
Hezekia akamwomba Bwana akisema:
16 [o]"Ee Bwana Mwenye Nguvu Zote, Mungu
wa Israeli, uketiye juu ya kiti cha enzi
kati ya makerubi, wewe peke yako ndiwe
Mungu juu ya falme zote za dunia. Wewe
umeumba mbingu na nchi. 17 [p]Tega sikio,
Ee Bwana, usikie; fungua macho yako, Ee
Bwana, uone; sikiliza maneno yote ambayo
Senakeribu ametuma kumtukana Mungu
aliye hai.

18 [q]"Ni kweli, Ee Bwana, kwamba
wafalme wa Ashuru wameyaangamiza
mataifa haya yote pamoja na nchi zao.

[a]**37:1** 2Nya 34:19; Mwa 37:34; 1Fal 8:33; Mt 21:13
[b]**37:2** 2Fal 22:14; Isa 13:1; 36:3; 2Fal 18:18
[c]**37:3** Isa 66:9; Hos 13:13; 2Fal 19:3; Amu 6:2; Isa 5:30; 26:18
[d]**37:4** Yak 5:14-15; Isa 36:13, 18-20; Amo 7:2; 2Nya 32:17; Yos 3:10; 1Sam 7:8
[e]**37:6** Yos 1:9; Isa 7:4; Hes 15:30
[f]**37:7** Isa 31:8; 1Nya 5:26
[g]**37:8** Hes 33:20; Neh 11:30; Yer 34:7; Yos 10:3
[h]**37:9** 2Nya 32:11; Isa 20:3
[i]**37:10** 2Nya 32:11, 15; Isa 36:15
[j]**37:11** Isa 36:18-20
[k]**37:12** Mwa 12:1-4; Mdo 7:2; 2Fal 18:11
[l]**37:13** Isa 10:9; 2Fal 17:24; Isa 36:20
[m]**37:14** 2Nya 32:17; 1Fal 8:33
[n]**37:15** 2Nya 32:20
[o]**37:16** Kum 10:17; Za 46:10; Kut 25:22; Mwa 3:24; Za 86:10; Dan 4:34; Mdo 4:24
[p]**37:17** Dan 9:18; Yer 25:29; 2Nya 6:40; 1Fal 8:29; 2Nya 32:17
[q]**37:18** 2Fal 15:29; Nah 2:11-12

19 [a]Wameitupa miungu yao kwenye moto na
kuiangamiza, kwa kuwa haikuwa miungu,
bali miti na mawe tu, iliyotengenezwa
kwa mikono ya wanadamu. 20 [b]Sasa basi,
Ee BWANA Mungu wetu, tuokoe kutoka
mkononi mwake, ili kwamba falme zote
duniani zipate kujua kwamba wewe peke
yako, Ee BWANA, ndiwe Mungu."

*Kuanguka Kwa Senakeribu*

**(2 Wafalme 19:20-37)**

21 [c]Kisha Isaya mwana wa Amozi
akapeleka ujumbe kwa Hezekia, akasema:
"Hili ndilo asemalo BWANA, Mungu wa
Israeli: Kwa sababu umeniomba kuhusu
Senakeribu mfalme wa Ashuru, 22 [d]hili ndilo
neno ambalo BWANA amelisema dhidi yake:

"Bikira binti Sayuni anakudharau na
kukudhihaki.
Binti Yerusalemu anatikisa kichwa
chake unapokimbia.
23 [e]Ni nani uliyemtukana na
kumkufuru?
Ni nani uliyeinua sauti yako dhidi
yake,
na kumwinulia macho yako kwa
kiburi?
Ni dhidi ya yule Aliye Mtakatifu
wa Israeli!
24 [f]Kupitia kwa wajumbe wako
umelundika matukano juu ya
Bwana.
Nawe umesema,
'Kwa magari yangu mengi ya vita,
nimepanda juu ya vilele vya milima,
vilele vya juu sana katika
Lebanoni.
Nami nimeiangusha mierezi yake
mirefu,
misunobari yake iliyo bora sana.
Nimefikia sehemu zake zilizoinuka
juu sana,
misitu yake iliyo mizuri sana.
25 [g]Nimechimba visima katika nchi za
kigeni
na kunywa maji yake.
Kwa nyayo za miguu yangu
nimekausha vijito vyote vya
Misri.'

26 [h]"Je, hujasikia?
Zamani sana niliamuru hili.
Siku za kale nilipanga hili;
sasa nimelifanya litokee,
kwamba umegeuza miji yenye
ngome
kuwa malundo ya mawe.
27 [i]Watu wa miji hiyo wameishiwa
nguvu,
wanavunjika mioyo na
kuaibishwa.
Wao ni kama mimea katika shamba,
kama machipukizi mororo ya
kijani,
kama majani yachipuayo juu ya paa
la nyumba,
ambayo hukauka kabla ya kukua.

28 [j]"Lakini ninajua mahali ukaapo,
kutoka kwako na kuingia kwako,
na jinsi unavyoghadhibika dhidi
yangu.
29 [k]Kwa sababu unaghadhibika na
ufidhuli dhidi yangu,
na kwa sababu ufidhuli wako
umefika masikioni mwangu,
nitaweka ndoana yangu puani
mwako
na hatamu yangu kinywani
mwako,
nami nitakufanya urudi kwa njia
ile uliyoijia.

[a]**37:19** Isa 36:20; Yer 2:11; Gal 4:8; Yos 7:15; Isa 26:14; 2Nya 13:9; Isa 40:18-20; 44:9-11
[b]**37:20** 1Sam 17:46; Za 46:10; Mit 20:22; Yos 4:24
[c]**37:21** Isa 37:2
[d]**37:22** Isa 23:12; 10:32; Ay 16:4
[e]**37:23** Hes 15:30; Dan 7:25; Isa 2:11; 52:5; Eze 36:20-23; Ay 15:25; Isa 12:6
[f]**37:24** Isa 14:8; 36:9; 1Fal 5:8-10; Isa 14:5, 13; 41:19; Hos 14:8
[g]**37:25** Kum 11:10; Dan 4:30; Isa 19:6; 44:27; 10:14
[h]**37:26** Mdo 4:27-28; 1Pet 2:8; Isa 25:1-2; Kum 13:16; Mdo 2:23; Isa 10:6
[i]**37:27** Isa 15:6; Za 129:6
[j]**37:28** Za 139:1-3; 2:1
[k]**37:29** Isa 10:12; Ay 41:2; 40:24; Eze 38:4; Amo 4:2; 2Nya 33:11

30 [a]“Hii ndiyo itakuwa ishara kwako, ee Hezekia:

“Mwaka huu utakula kile kiotacho
chenyewe,
na mwaka wa pili utakula kutoka
machipukizi yake.
Lakini katika mwaka wa tatu panda
na uvune,
panda mashamba ya mizabibu na
ule matunda yake.
31 [b]Mara nyingine tena mabaki ya
nyumba ya Yuda
wataeneza mizizi chini na kuzaa
matunda juu.
32 [c]Kwa kuwa kutoka Yerusalemu
watakuja mabaki,
na kutoka Mlima Sayuni kundi la
walionusurika.
Wivu wa BWANA Mwenye Nguvu
Zote,
ndio utatimiza jambo hili.

33 [d]“Kwa hiyo hili ndilo asemalo BWANA kuhusu mfalme wa Ashuru:

“Hataingia katika mji huu
wala hatapiga mshale hapa.
Hatakuja mbele yake na ngao
wala kupanga majeshi kuuzingira.
34 [e]Kwa njia ile aliyoijia ndiyo
atakayorudi;
hataingia katika mji huu,”
asema BWANA.
35 [f]“Nitaulinda mji huu na kuuokoa,
kwa ajili yangu mwenyewe,
na kwa ajili ya Daudi mtumishi
wangu!”

36 [g]Ndipo malaika wa BWANA akaenda,
akawaua wanajeshi 185,000 katika kambi
ya Waashuru. Wenzao walipoamka asubuhi
yake, walikuta maiti kila mahali!
37 [h]Basi
Senakeribu mfalme wa Ashuru akavunja
kambi na kuondoka. Akarudi Ninawi na
kukaa huko.
38 [i]Siku moja, alipokuwa akiabudu katika
hekalu la mungu wake Nisroki, wanawe
Adrameleki na Shareza wakamuua kwa
upanga, nao wakakimbilia nchi ya Ararati.
Naye Esar-Hadoni mwanawe akawa mfalme
badala yake.

*Kuugua Kwa Mfalme Hezekia*

**(2 Wafalme 20:1-11; 2 Nyakati 32:24-26)**

38 [j]Katika siku hizo Hezekia akaugua,
naye akawa karibu kufa. Nabii Isaya
mwana wa Amozi akaenda kwake na
kumwambia, “Hili ndilo asemalo BWANA:
Tengeneza mambo ya nyumba yako, kwa
sababu utakufa, hutapona.”
2 Hezekia akaelekeza uso wake ukutani,
akamwomba BWANA:
3 [k]“Ee BWANA,
kumbuka jinsi nilivyoenenda mbele zako
kwa uaminifu na kujitoa kwa moyo wangu
wote, na kufanya yaliyo mema machoni
pako.” Naye Hezekia akalia kwa uchungu.
4 [l]Ndipo neno la BWANA likamjia Isaya,
kusema:
5 [m]“Nenda ukamwambie Hezekia,
‘Hili ndilo asemalo BWANA, Mungu wa baba
yako Daudi: Nimeyasikia maombi yako na
nimeona machozi yako. Nitakuongezea
miaka kumi na mitano katika maisha yako.
6 [n]Nami nitakuokoa wewe pamoja na mji
huu mkononi mwa mfalme wa Ashuru.
Nitaulinda mji huu.
7 [o]‘Hii ndiyo ishara ya BWANA kwako ya
kwamba BWANA atafanya kile alichoahidi:
8 [p]Nitafanya kivuli cha jua kwenye ngazi
iliyojengwa na Ahazi kirudi nyuma

[a]**37:30** Isa 20:3; 32:10; 16:14; Law 25:4; Yer 31:5; Za 107:37
[b]**37:31** Isa 27:6; 11:10
[c]**37:32** Isa 11:11; 1:9; 9:7
[d]**37:33** Isa 32:18; 2Sam 20:15
[e]**37:34** Isa 37:29
[f]**37:35** Isa 31:5; 38:6; Eze 48:9-11; 36:21-22; 2Fal 20:6; 1Nya 17:19
[g]**37:36** Kut 12:12, 23; Isa 10:12
[h]**37:37** Mwa 10:11; Nah 1:1; 2Nya 32:1
[i]**37:38** Mwa 8:4; Yer 51:27; 2Fal 17:24; Isa 14:25; 9:4; 10:26
[j]**38:1** Isa 37:2-3; 2Sam 17:23; 2Fal 8:10
[k]**38:3** Neh 5:19; 13:14; Kum 6:18; Za 26:3; 1Fal 8:61; 2Nya 29:19; Za 6:8
[l]**38:4** 1Sam 13:13; Isa 39:5
[m]**38:5** 2Fal 18:2-3; Za 6:6
[n]**38:6** Isa 31:5; 37:35
[o]**38:7** Mwa 24:14; 2Fal 20:8; 2Nya 32:31; Isa 7:11, 14; 20:3
[p]**38:8** Yos 10:13

madaraja kumi.' " Hivyo jua likarudi nyuma
madaraja kumi ambayo lilikuwa limeshuka.

9 Maandiko ya Hezekia mfalme wa Yuda
baada ya kuugua kwake na kupona:

10 [a]Nilisema, "Katika ustawi wa maisha yangu,
je, ni lazima nipite katika malango ya mauti,[b]
na kupokonywa miaka yangu iliyobaki?"
11 [c]Nilisema, "Sitamwona tena BWANA,
BWANA katika nchi ya walio hai,
wala sitamtazama tena mwanadamu,
wala kuwa na wale ambao sasa wanakaa katika ulimwengu huu.
12 [d]Kama hema la mchunga mifugo,
nyumba yangu imebomolewa na kutwaliwa kutoka kwangu.
Kama mfumaji nimevingirisha maisha yangu,
naye amenikatilia mbali kutoka kitanda cha mfumi.
Mchana na usiku uliyakomesha maisha yangu.
13 [e]Nilingoja kwa uvumilivu hadi mapambazuko,
lakini alivunja mifupa yangu yote kama simba.
Mchana na usiku uliyakomesha maisha yangu.
14 [f]Nililia kama mbayuwayu au korongo,
niliomboleza kama hua aombolezaye.
Macho yangu yalififia nilipotazama mbinguni.
Ee Bwana, ninataabika, njoo unisaidie!"
15 [g]Lakini niseme nini?
Amesema nami, naye yeye mwenyewe amelitenda hili.
Nitatembea kwa unyenyekevu katika miaka yangu yote
kwa sababu ya haya maumivu makali
ya nafsi yangu.
16 [h]Bwana, kwa mambo kama haya watu huishi,
nayo roho yangu hupata uzima katika hayo pia.
Uliniponya
na kuniacha niishi.
17 [i]Hakika ilikuwa ya faida yangu
ndiyo maana nikapata maumivu makali.
Katika upendo wako ukaniokoa
kutoka shimo la uharibifu;
umeziweka dhambi zangu zote
nyuma yako.
18 [j]Kwa maana kaburi[k] haliwezi kukusifu,
mauti haiwezi kuimba sifa zako;
wale washukao chini shimoni
hawawezi kuutarajia uaminifu wako.
19 [l]Walio hai, walio hai: hao wanakusifu,
kama ninavyofanya leo.
Baba huwaambia watoto wao
habari za uaminifu wako.

20 [m]BWANA ataniokoa,
nasi tutaimba kwa vyombo vya nyuzi
siku zote za maisha yetu
katika Hekalu la BWANA.

---

[a]**38:10** Ay 17:16; Za 102:24; 2Kor 1:9; Ay 17:11; Za 107:18
[b]10 Mauti hapa maana yake ni Kuzimu.
[c]**38:11** Za 27:13; Ay 28:13; 35:14; Isa 12:2; Za 116:5
[d]**38:12** 2Kor 5:4; Ay 4:21; Isa 33:20; Ebr 1:12; Hes 11:15; Za 32:4; 1Pet 1:13-14
[e]**38:13** Ay 9:17; Mao 3:4; Yer 34:17; Za 37:7; 51:8; Ay 10:16; Dan 6:24
[f]**38:14** Isa 59:11; Mwa 50:24; Ay 17:3; Mwa 8:8; Za 6:7
[g]**38:15** Ay 7:11; 1Fal 21:27; Za 39:9; 2Sam 7:20
[h]**38:16** Ebr 12:9; Za 119:25
[i]**38:17** Yer 31:34; Mik 7:19; Ay 17:16; Za 103:3, 12; Rum 8:28; Ebr 12:11; Isa 43:25
[j]**38:18** Mhu 9:10; Hes 16:30; Za 6:5; 30:9; 88:10-11; 115:17
[k]18 Kaburini hapa maana yake ni Kuzimu, kwa Kiebrania ni Sheol.
[l]**38:19** Kum 6:7; 11:19; Za 78:3; 118:7; 119:175
[m]**38:20** Za 68:25; 9:13; 45:8; 116:17-19; 63:4; 23:6

21 Isaya alikuwa amesema, "Tengenezeni
dawa ya kubandika ya tini, mweke juu ya
jipu, naye atapona."
22 Hezekia alikuwa ameuliza, "Kutakuwa
na ishara gani kwamba nitapanda kwenda
Hekalu la BWANA?"

*Wajumbe Kutoka Babeli*

**(2 Wafalme 20:12-19)**

39 [a]Wakati huo Merodaki-Baladani,
mwana wa Baladani mfalme wa Babeli,
akamtumia Hezekia barua na zawadi,
kwa sababu alikuwa amesikia habari za
kuugua na kupona kwake.
2 [b]Hezekia
akawapokea wale wajumbe kwa furaha
na kuwaonyesha vitu vile vilivyokuwa
katika ghala zake: yaani fedha, dhahabu,
vikolezo na mafuta safi, ghala la silaha lote,
na kila kitu kilichokuwa katika hazina zake.
Hapakuwa na kitu chochote katika jumba
lake la kifalme au katika ufalme wake wote
ambacho Hezekia hakuwaonyesha.
3 [c]Ndipo nabii Isaya akaenda kwa Mfalme
Hezekia na kumuuliza, "Watu hao walisema
nini, na wametoka wapi?"
Hezekia akamjibu, "Wametoka nchi ya
mbali. Walikuja kwangu kutoka Babeli."
4 Nabii akauliza, "Waliona nini katika
jumba lako la kifalme?"
Hezekia akajibu, "Waliona kila kitu
katika jumba langu la kifalme. Hakuna
kitu chochote katika hazina yangu ambacho
sikuwaonyesha."
5 [d]Ndipo Isaya akamwambia Hezekia,
"Sikia neno la BWANA Mwenye Nguvu
Zote:
6 [e]Hakika wakati unakuja ambapo vitu
vyote katika jumba lako la kifalme, na vyote
ambavyo baba zako waliweka akiba mpaka
siku hii, vitachukuliwa kwenda Babeli.
Hakuna chochote kitakachosalia, asema
BWANA.
7 [f]Nao baadhi ya wazao wako,
nyama yako na damu yako mwenyewe
watakaozaliwa kwako, watachukuliwa
mbali, nao watakuwa matowashi katika
jumba la mfalme wa Babeli."
8 [g]Hezekia akamjibu Isaya, "Neno la
BWANA ulilosema ni jema." Kwa kuwa
alifikiri, "Patakuwepo amani na usalama
wakati wa uhai wangu."

*Faraja Kwa Watu Wa Mungu*

40 [h]Wafarijini, wafarijini watu
wangu,
asema Mungu wenu.
2 [i]Sema na Yerusalemu kwa upole,
umtangazie
kwamba kazi yake ngumu
imekamilika,
kwamba dhambi yake imefanyiwa
fidia,
kwamba amepokea kutoka mkononi
mwa BWANA
maradufu kwa ajili ya dhambi
zake zote.

3 [j]Sauti ya mtu aliaye:
"Itengenezeni jangwani njia ya
BWANA,
nyoosheni njia kuu nyikani
kwa ajili ya Mungu wetu.
4 [k]Kila bonde litainuliwa,
kila mlima na kilima kitashushwa;
penye mabonde patanyooshwa,
napo palipoparuza
patasawazishwa.
5 [l]Utukufu wa BWANA utafunuliwa,
nao wanadamu wote watauona
pamoja.
Kwa maana kinywa cha BWANA
kimenena."

---

[a]**39:1** 2Fal 20:12; 2Nya 32:31
[b]**39:2** 2Nya 32:31; 2Fal 18:15; 2Nya 32:27-29
[c]**39:3** Kum 28:49
[d]**39:5** Isa 38:4
[e]**39:6** Law 26:33; Amu 6:4; Yer 20:5; Amo 5:27; 2Fal 24:13
[f]**39:7** 2Fal 24:15; Dan 1:1-7
[g]**39:8** 1Sam 3:18; 2Nya 32:26; Amu 10:15; Ay 1:21; Za 39:9
[h]**40:1** Zek 1:17; 2Kor 1:3; Sef 3:14-17; Yer 31:13; Isa 49:13; 57:18
[i]**40:2** Mwa 34:3; Isa 41:11-13; 49:25; Zek 9:12; Ufu 18:6; Yer 16:18; Law 26:4
[j]**40:3** Isa 11:16; Mt 3:3; Mal 3:1; Mk 1:3; Isa 43:19; Yn 1:23
[k]**40:4** Za 26:12; Yer 31:9; Isa 2:14; 49:11; 26:7; 45:2
[l]**40:5** Kut 16:7; Isa 58:14; Lk 3:4-6; Eze 36:23; Hes 14:21; Isa 59:19; Lk 2:20

6 [a]Sauti husema, “Piga kelele.”
Nami nikasema, “Nipige kelele gani?”

“Wanadamu wote ni kama majani,
nao utukufu wao wote
ni kama maua ya kondeni.
7 [b]Majani hunyauka na maua huanguka,
kwa sababu pumzi ya BWANA huyapuliza.
Hakika wanadamu ni majani.
8 [c]Majani hunyauka na maua huanguka,
lakini neno la Mungu wetu ladumu milele.”

9 [d]Wewe uletaye habari njema Sayuni,
panda juu ya mlima mrefu.
Wewe uletaye habari njema Yerusalemu,
inua sauti yako kwa kupiga kelele,
inua sauti, usiogope;
iambie miji ya Yuda,
“Yuko hapa Mungu wenu!”
10 [e]Tazameni, BWANA Mwenyezi anakuja na nguvu,
nao mkono wake ndio utawalao kwa ajili yake.
Tazameni, ujira wake u pamoja naye,
nayo malipo yake yanafuatana naye.
11 [f]Huchunga kundi lake kama mchungaji wa mifugo:
Hukusanya wana-kondoo katika mikono yake
na kuwachukua karibu na moyo wake,
huwaongoza taratibu wale wanyonyeshao.

12 [g]Ni nani aliyepima maji ya bahari kwenye konzi ya mkono wake,
au kuzipima mbingu kwa shibiri[h] yake?
Ni nani aliyeyashika mavumbi ya dunia katika kikapu,
au kupima milima kwenye kipimio
na vilima kwenye mizani?
13 [i]Ni nani aliyeyafahamu mawazo ya BWANA,
au kumfundisha akiwa kama mshauri wake?
14 [j]Ni nani ambaye BWANA ametaka shauri kwake ili kumwelimisha,
naye ni nani aliyemfundisha njia iliyo sawa?
Ni nani aliyemfundisha maarifa
au kumwonyesha mapito ya ufahamu?

15 [k]Hakika mataifa ni kama tone ndani ya ndoo,
ni kama vumbi jembamba juu ya mizani,
huvipima visiwa kana kwamba vilikuwa vumbi laini.
16 [l]Lebanoni hautoshi kwa moto wa madhabahuni,
wala wanyama wake hawatoshi kwa sadaka za kuteketezwa.
17 [m]Mbele yake mataifa yote ni kama si kitu,
yanaonekana yasio na thamani
na zaidi ya bure kabisa.

18 [n]Basi, utamlinganisha Mungu na nani?
Utamlinganisha na kitu gani?

[a]**40:6** Ay 14:2; Mwa 6:3; Isa 29:5
[b]**40:7** Kut 15:10; Ay 41:21; Yos 8:12; Isa 15:6; Za 103:6; Eze 22:21
[c]**40:8** 1Pet 1:25; Isa 59:21; Mt 5:18; Za 119:89; Isa 5:24; Yak 1:10; Mit 19:21
[d]**40:9** Nah 1:15; Isa 25:9; Rum 10:15; Isa 41:27; 52:7-10; 1Kor 15:1-4
[e]**40:10** Ufu 22:7; Isa 35:4; Za 44:3; Isa 9:6-7; Ufu 22:12; Mt 21:5; Isa 28:2
[f]**40:11** Za 28:9; Yn 10:11; Ebr 13:20; Mwa 48:15; Mik 5:4; Hes 12:11; Kum 26:19
[g]**40:12** Mit 30:4; Ebr 1:10-12; Ay 38:10; 12:15; Mit 16:11
[h]12 Shibiri ni sawa na sentimita 20 au inchi 8.
[i]**40:13** Ay 15:8; 1Kor 2:16; Rum 11:34
[j]**40:14** Ay 21:22; Kol 2:3; Ay 12:13; 34:13; Isa 55:9
[k]**40:15** Za 62:9; Isa 2:22; Kum 9:21
[l]**40:16** Mik 6:7; Ebr 10:5-9; Isa 37:24; Za 50:9-11
[m]**40:17** Isa 30:28; Ay 12:19; Isa 29:7; Dan 4:35; Isa 37:19
[n]**40:18** Mdo 17:29; Kut 8:10; Kum 4:15; 1Sam 2:2

19 [a]Kwa habari ya sanamu, fundi
huisubu,
naye mfua dhahabu huifunika kwa
dhahabu
na kuitengenezea mikufu ya fedha.
20 [b]Mtu aliye maskini sana asiyeweza
kuleta sadaka kama hii
huuchagua mti usiooza.
Humtafuta fundi stadi
wa kusimamisha sanamu ambayo
haitatikisika.

21 [c]Je, hujui?
Je, hujasikia?
Je, hujaambiwa tangu mwanzo?
Je, hujafahamu tangu kuumbwa
kwa dunia?
22 [d]Anakaa kwenye kiti cha enzi juu ya
duara ya dunia,
nao watu wakaao ndani yake ni
kama panzi.
Huzitandaza mbingu kama
chandarua,
na kuzitandaza kama hema la
kuishi.
23 [e]Huwafanya wakuu kuwa si kitu,
na kuwashusha watawala wa
dunia hii kuwa kitu bure.
24 [f]Mara baada ya kupandwa,
mara baada ya kutiwa ardhini,
mara baada ya kutoa mizizi yao
ardhini,
ndipo huwapulizia nao wakanyauka,
nao upepo wa kisulisuli
huwapeperusha kama makapi.

25 [g]"Utanilinganisha mimi na nani?
Au ni nani anayelingana nami?"
asema yeye Aliye Mtakatifu.
26 [h]Inueni macho yenu mtazame
mbinguni:
Ni nani aliyeumba hivi vyote?
Ni yeye aletaye nje jeshi la nyota
moja baada ya nyingine
na kuziita kila moja kwa jina lake.
Kwa sababu ya uweza wake mkuu na
nguvu zake kuu,
hakuna hata mojawapo
inayokosekana.

27 [i]Kwa nini unasema, ee Yakobo,
nanyi ee Israeli, kulalamika,
"Njia yangu imefichwa Bwana
asiione,
Mungu wangu hajali shauri
langu?"
28 [j]Je wewe, hufahamu?
Je wewe, hujasikia?
Bwana ni Mungu wa milele,
Muumba wa miisho ya dunia.
Hatachoka wala kulegea,
wala hakuna hata mmoja
awezaye kuupima ufahamu wake.
29 [k]Huwapa nguvu waliolegea
na huongeza nguvu za wadhaifu.
30 [l]Hata vijana huchoka na kulegea,
nao vijana wanaume hujikwaa na
kuanguka,
31 [m]bali wale wamtumainio Bwana
atafanya upya nguvu zao.
Watapaa juu kwa mbawa kama tai;
watapiga mbio wala hawatachoka,
watatembea kwa miguu wala
hawatazimia.

[a]**40:19** Kut 20:4; Zek 10:2; Yer 10:3-4; Isa 31:7; 37:19; 42:17; Hab 2:18
[b]**40:20** Isa 44:19; 5:3
[c]**40:21** Mdo 14:17; Rum 1:19; Isa 48:13; 51:13; 2Fal 19:25
[d]**40:22** Hes 13:33; Ay 22:14; 36:29; 2Nya 6:18; Isa 48:13; Ay 26:7
[e]**40:23** Ay 12:18; Isa 34:12; Za 107:40; Amo 2:3
[f]**40:24** 2Sam 22:16; Isa 11:4; Ay 5:3; 8:12; 18:16; 24:24; Isa 41:2, 16
[g]**40:25** Kum 4:15; Mdo 17:24-29; 1Nya 16:25; Isa 37:23
[h]**40:26** Za 89:11-13; 2Fal 17:16; Neh 9:6; Isa 34:16; 51:6; Ay 9:4; Efe 1:19
[i]**40:27** Ay 6:29; Lk 18:7-8; Ay 27:2
[j]**40:28** Kum 33:27; Za 90:2; Rum 11:33; Isa 37:16; 44:12; Za 147:5
[k]**40:29** Isa 57:19; Yer 31:25; Mwa 18:14; Za 68:35; 119:28
[l]**40:30** Isa 9:17; Yer 9:21; Isa 5:27
[m]**40:31** 2Fal 6:33; Kut 19:4; Ebr 12:1-3; Mao 3:25; 2Kor 4:8-10, 16; Za 37:9; Isa 30:18

*Msaidizi Wa Israeli*

41 [a]“Nyamazeni kimya mbele zangu,
enyi visiwa!
Mataifa na wafanye upya nguvu
zao!
Wao na wajitokeze, kisha waseme,
tukutane pamoja mahali pa
hukumu.

2 [b]“Ni nani aliyemchochea mmoja
kutoka mashariki,
akimwita katika haki kwa
utumishi wake?
Huyatia mataifa mikononi mwake,
na kuwatiisha wafalme mbele
zake.
Huwafanya kuwa mavumbi kwa
upanga wake,
huwafanya makapi
yapeperushwayo na upepo
kwa upinde wake.
3 [c]Huwafuatia na kuendelea salama,
katika njia ambayo miguu yake
haijawahi kupita.
4 [d]Ni nani aliyefanya jambo hili na
kulitimiliza,
akiita vizazi tangu mwanzo?
Mimi, Bwana, ni wa kwanza
nami nitakuwa pamoja na wa
mwisho:
mimi Bwana ndiye.”

5 [e]Visiwa vimeliona na kuogopa,
miisho ya dunia inatetemeka.
Wanakaribia na kuja mbele,
6 [f]kila mmoja humsaidia mwingine
na kusema kwa ndugu yake, “Uwe
hodari!”
7 [g]Fundi humtia moyo sonara,
yeye alainishaye kwa nyundo
humhimiza yeye agongeaye
kwenye fuawe,
Humwambia yeye aunganishaye, “Ni
kazi njema.”
Naye huikaza sanamu kwa
misumari ili isitikisike.

8 [h]“Lakini wewe, ee Israeli, mtumishi
wangu,
Yakobo, niliyemchagua,
ninyi wazao wa Abrahamu rafiki
yangu,
9 [i]nilikuchukua toka miisho ya dunia,
nilikuita kutoka pembe zake za
mbali.
Nilisema, ‘Wewe ni mtumishi
wangu’;
nimekuchagua, wala sikukukataa.
10 [j]Hivyo usiogope, kwa maana niko
pamoja nawe;
usifadhaike, kwa maana mimi ni
Mungu wako.
Nitakutia nguvu na kukusaidia;
nitakutegemeza kwa mkono wa
kuume wa haki yangu.

11 [k]“Wote walioona hasira dhidi yako
hakika wataaibika na
kutahayarika,
wale wakupingao
watakuwa kama vile si kitu, na
kuangamia.
12 [l]Ingawa utawatafuta adui zako,
hutawaona.
Wale wanaopigana vita dhidi yako
watakuwa kama vile si kitu kabisa.
13 [m]Kwa maana Mimi ndimi Bwana,
Mungu wako,
nikushikaye mkono wako wa
kuume
na kukuambia, Usiwe na hofu,
nitakusaidia.

---

[a]**41:1** Za 37:7; Isa 48:16; 50:8; Hab 2:20; Zek 2:13; Isa 11:11; 1Sam 2:4
[b]**41:2** 2Sam 22:43; Isa 40:24; Yer 51:11; Ezr 1:2; Isa 44:28; Yer 50:3; 25:9
[c]**41:3** Dan 8:4
[d]**41:4** Isa 48:12; Ufu 22:13; Mdo 15:18; Isa 43:7; Kum 32:29
[e]**41:5** Eze 26:17-18; Kum 30:4; Isa 11:11-12
[f]**41:6** Isa 1:6
[g]**41:7** Isa 40:19; 44:13; Yer 30:3-5
[h]**41:8** Mwa 18:19; Isa 29:22; Neh 9:7; 2Nya 20:7; Yak 2:23; Isa 63:16; Za 136:22
[i]**41:9** Isa 37:16; Kum 7:6; Isa 20:3; 11:12
[j]**41:10** Kum 3:22; Rum 8:3; Isa 49:8; Yer 30:10; 46:27-28; Ay 40:14; Za 18:35
[k]**41:11** Isa 17:12; 54:17; Kut 23:22; Isa 29:8; Zek 12:3; Yer 2:3; Isa 29:23
[l]**41:12** Za 37:35-36; Isa 34:12; Ay 7:8; Isa 29:20; 17:14
[m]**41:13** Za 73:23; Isa 42:6; 45:1; 51:18

14 [a]Usiogope, ee Yakobo uliye mdudu,
ee Israeli uliye mdogo,
kwa kuwa Mimi mwenyewe
nitakusaidia," asema BWANA,
Mkombozi wako, yeye Aliye
Mtakatifu wa Israeli.
15 [b]"Tazama, nitakufanya chombo cha
kupuria,
kipya na chenye makali, chenye
meno mengi.
Utaipura milima na kuiponda
na kuvifanya vilima kuwa kama
makapi.
16 [c]Utaipepeta, nao upepo utaichukua,
dhoruba itaipeperushia mbali.
Bali wewe utajifurahisha katika
BWANA
na katika utukufu wa yeye Aliye
Mtakatifu wa Israeli.

17 [d]"Maskini na wahitaji wanatafuta
maji,
lakini hayapo,
ndimi zao zimekauka kwa kiu.
Lakini Mimi BWANA nitawajibu,
Mimi, Mungu wa Israeli,
sitawaacha.
18 [e]Nitaifanya mito itiririke juu ya
vilima vilivyo kame,
nazo chemchemi ndani ya
mabonde.
Nitaligeuza jangwa liwe mabwawa
ya maji,
nayo ardhi iliyokauka kuwa
chemchemi za maji.
19 [f]Katika jangwa nitaotesha
mwerezi, mshita, mhadasi na
mzeituni.
Nitaweka misunobari, mivinje na
misanduku
pamoja huko nyikani,
20 [g]ili kwamba watu wapate kuona na
kujua,
wapate kufikiri na kuelewa,
kwamba mkono wa BWANA
umetenda hili,
kwamba yeye Aliye Mtakatifu wa
Israeli ndiye alilifanya."

21 [h]BWANA asema, "Leta shauri lako.
Toa hoja yako," asema Mfalme wa
Yakobo.
22 [i]"Leteni sanamu zenu zituambie
ni nini kitakachotokea.
Tuambieni mambo ya zamani
yalikuwa nini,
ili tupate kuyatafakari
na kujua matokeo yake ya
mwisho.
Au tutangazieni mambo
yatakayokuja,
23 [j]tuambieni ni nini kitakachotokea
baadaye,
ili tupate kujua kuwa ninyi ni
miungu.
Fanyeni jambo lolote zuri au baya,
ili tupate kutishika na kujazwa na
hofu.
24 [k]Lakini ninyi ni zaidi ya bure kabisa,
na kazi zenu hazifai kitu kabisa;
yeye awachaguaye ni chukizo
sana.

25 [l]"Nimemchochea mtu mmoja kutoka
kaskazini,
naye yuaja, mmoja toka mawio ya
jua aliitaye Jina langu.

[a]**41:14** Ay 4:19; Za 22:6; Kut 15:13; Ay 19:23; Isa 1:27
[b]**41:15** Ay 41:30; Mik 4:13; Isa 21:10; Kut 19:18; Yer 9:10; Eze 33:28
[c]**41:16** Yer 51:2; Isa 45:25; 60:19; Dan 2:35; Yer 15:7; Isa 25:9; Mk 1:24
[d]**41:17** Isa 43:20; 35:7; 30:19
[e]**41:18** Isa 30:25; 43:19; Ay 38:26; Isa 35:7; 2Fal 3:17
[f]**41:19** Isa 60:13; Kut 25:10-13; Isa 37:24; 44:14
[g]**41:20** Ay 12:9; Isa 4:5
[h]**41:21** Isa 43:14; 44:6
[i]**41:22** Isa 48:14; 65:17; Yn 13:19; Isa 43:9; 45:21
[j]**41:23** Kum 18:22; Isa 44:7-8; Yer 10:5; Isa 43:5; 2Fal 19:26
[k]**41:24** Isa 37:19; 1Kor 8:4; Za 115:8; 1Sam 12:21; Isa 48:8
[l]**41:25** Yer 51:48; Nah 3:14; 2Sam 22:43; Yer 50:9

Huwakanyaga watawala kana
kwamba ni matope,
kama mfinyanzi akanyagavyo
udongo wa kufinyangia.
26 [a]Ni nani aliyenena hili tokea
mwanzoni, ili tupate kujua,
au kabla, ili tuweze kusema,
'Alikuwa sawa'?
Hakuna aliyenena hili,
hakuna aliyetangulia kusema hili,
hakuna yeyote aliyesikia maneno
kutoka kwenu.
27 [b]Nilikuwa wa kwanza kumwambia
Sayuni,
'Tazama, wako hapa!'
Nilimpa Yerusalemu mjumbe wa
habari njema.
28 [c]Ninatazama, lakini hakuna yeyote:
hakuna yeyote miongoni mwao
awezaye kutoa shauri,
hakuna yeyote wa kutoa jibu
wakati ninapowauliza.
29 [d]Tazama, wote ni ubatili!
Matendo yao ni bure;
vinyago vyao ni upepo mtupu na
machafuko.

*Mtumishi Wa Bwana*

42 [e]"Huyu hapa mtumishi wangu,
ninayemtegemeza,
mteule wangu, ambaye
ninapendezwa naye;
nitaweka Roho yangu juu yake,
naye ataleta haki kwa mataifa.
2 [f]Hatapaza sauti wala kupiga kelele,
wala hataiinua sauti yake
barabarani.
3 [g]Mwanzi uliopondeka hatauvunja,
na utambi unaofuka moshi
hatauzima.
Kwa uaminifu ataleta haki,
4 [h]hatazimia roho wala kukata
tamaa,
mpaka atakaposimamisha haki juu
ya dunia.
Visiwa vitaweka tumaini lao
katika sheria yake."

5 [i]Hili ndilo asemalo Mungu, Bwana,
yeye aliyeziumba mbingu na
kuzitanda,
aliyeitandaza dunia na vyote
vitokavyo humo,
awapaye watu wake pumzi,
na uzima kwa wale waendao
humo:
6 [j]"Mimi, Bwana, nimekuita katika
haki;
nitakushika mkono wako.
Nitakulinda na kukufanya
kuwa Agano kwa ajili ya watu
na nuru kwa Mataifa,
7 [k]kuwafungua macho wale wasioona,
kuwaacha huru kutoka kifungoni
waliofungwa jela,
na kuwafungua kutoka gerezani
wale wanaokaa gizani.

8 [l]"Mimi ndimi Bwana; hilo ndilo Jina
langu!
Sitampa mwingine utukufu wangu
wala sanamu sifa zangu.
9 [m]Tazama, mambo ya kwanza
yametokea,
nami natangaza mambo mapya;
kabla hayajatokea
nawatangazia habari zake."

[a]**41:26** Hab 2:18-19; 1Fal 18:26; Isa 52:6
[b]**41:27** Isa 48:3, 16; 40:9
[c]**41:28** Eze 22:30; Za 22:11; Isa 40:13-14; 50:2; 59:16; 64:7; Yer 25:4
[d]**41:29** Yer 5:13; 1Sam 12:21; Isa 37:19
[e]**42:1** Isa 49:3-6; 14:1; Yn 3:34; Lk 9:35; Mwa 49:10; Mt 3:16-17; 20:28
[f]**42:2** Za 8:1-4
[g]**42:3** Za 72:2; Mt 12:17-21; Za 96:13; Isa 36:6; Ay 30:24; 13:25
[h]**42:4** Mwa 49:10; Ebr 12:2; Rum 8:22-25; Kut 34:29; Isa 51:4; 11:11
[i]**42:5** Za 24:2; Mdo 17:24-25; Isa 44:24; 48:13; Za 102:25
[j]**42:6** Kut 31:2; Amu 4:10; Yer 23:6; Mdo 13:47; Dan 9:7; Isa 26:18; Lk 22:20
[k]**42:7** Zek 9:11; 2:7; 2Tim 2:26; Lk 4:19; Mt 11:5; Isa 32:3; 51:14; Za 146:8
[l]**42:8** Kut 3:14-15; 6:3; Isa 48:11; Za 81:10; Ebr 2:14-15; Kut 8:10; Isa 46:9
[m]**42:9** Isa 41:22; 40:21; Eze 2:4

*Wimbo Wa Kumsifu* Bwana

10 [a]Mwimbieni Bwana wimbo mpya,
sifa zake toka miisho ya dunia,
ninyi mshukao chini baharini,
na vyote vilivyomo ndani yake,
enyi visiwa na wote wakaao ndani yake.
11 [b]Jangwa na miji yake na vipaze sauti zao;
makao anamoishi Kedari na yashangilie.
Watu wa Sela waimbe kwa furaha,
na wapige kelele kutoka vilele vya milima.
12 [c]Wampe Bwana utukufu,
na kutangaza sifa zake katika visiwa.
13 [d]Bwana ataenda kama mtu mwenye nguvu,
kama shujaa atachochea shauku yake,
kwa kelele ataamsha kilio cha vita,
naye atashinda adui zake.

14 [e]"Kwa muda mrefu nimenyamaza kimya,
nimekaa kimya na kujizuia.
Lakini sasa, kama mwanamke wakati wa kujifungua,
ninapiga kelele, ninatweta na kushusha pumzi.
15 [f]Nitaharibu milima na vilima
na kukausha mimea yako yote;
nitafanya mito kuwa visiwa
na kukausha mabwawa.
16 [g]Nitawaongoza vipofu kwenye njia ambayo hawajaijua,
kwenye mapito wasiyoyazoea nitawaongoza;
nitafanya giza kuwa nuru mbele yao,
na kufanya mahali palipoparuza kuwa laini.
Haya ndiyo mambo nitakayofanya;
mimi sitawaacha.
17 [h]Lakini wale wanaotumaini sanamu,
wanaoviambia vinyago, 'Ninyi ndio miungu yetu,'
watarudishwa nyuma kwa aibu kubwa.

*Israeli Kipofu Na Kiziwi*

18 "Sikieni, enyi viziwi;
tazameni, enyi vipofu, mpate kuona!
19 [i]Ni nani aliye kipofu isipokuwa mtumishi wangu,
na kiziwi kama mjumbe ninayemtuma?
Ni nani aliye kipofu kama yeye aliyejitoa kwangu,
aliye kipofu kama mtumishi wa Bwana?
20 [j]Mmeona vitu vingi, lakini hamkuzingatia;
masikio yenu yako wazi, lakini hamsikii chochote."

21 [k]Ilimpendeza Bwana
kwa ajili ya haki yake
kufanya sheria yake kuwa kuu na tukufu.
22 [l]Lakini hili ni taifa lililoibwa na kutekwa nyara,
wote wamenaswa katika mashimo,
au wamefichwa katika magereza.

---

[a]**42:10** Za 98:1; Kum 30:4; Za 96:11; 1Fal 10:9; 1Nya 16:32; Za 48:10; Isa 11:11
[b]**42:11** Mwa 25:13; Isa 32:16; 52:7; Nah 1:15; Isa 60:7; Amu 1:36
[c]**42:12** Isa 24:15; 1Nya 16:24; 1Pet 2:9; Za 26:7; 66:2
[d]**42:13** Isa 9:6; Yos 6:5; Yoe 3:16; Isa 66:14; 26:11; Kut 14:14; Hos 11:10
[e]**42:14** Es 4:14; Yer 4:31; Mwa 43:31; Lk 18:7
[f]**42:15** Eze 38:20; Za 107:33; Isa 11:15; 50:2; Nah 1:4-6
[g]**42:16** Kum 4:31; Ebr 13:5; Yer 31:8-9; Isa 26:7; 29:24; 57:18; Mdo 26:18; Ebr 13:5
[h]**42:17** Kut 32:4; Za 97:7; Isa 1:26
[i]**42:19** Isa 43:8; Eze 12:2; Isa 41:8-9; Hag 1:13; Isa 26:3
[j]**42:20** Isa 6:9-10; Yer 5:21; Rum 2:21; Yer 6:10; Isa 48:21; 41:17
[k]**42:21** 2Kor 3:7; Isa 43:25
[l]**42:22** Isa 24:18-22; Lk 19:41-44; Amu 6:4; 2Fal 24:13; Isa 5:29; Za 66:11; Yos 22:5; Isa 1:14; 30:11

Wamekuwa nyara,
wala hapana yeyote awaokoaye.
Wamefanywa mateka,
wala hapana yeyote asemaye,
"Warudishe."

23 [a]Ni nani miongoni mwenu
atakayesikiliza hili,
au atakayezingatia kwa makini
katika wakati ujao?
24 [b]Ni nani aliyemtoa Yakobo kuwa
mateka,
na Israeli kwa wateka nyara?
Je, hakuwa yeye, BWANA,
ambaye tumetenda dhambi dhidi
yake?
Kwa kuwa hawakufuata njia zake,
hawakutii sheria zake.
25 [c]Hivyo akawamwagia hasira yake
inayowaka,
ukali wa vita.
Iliwazunguka kwa miali ya
moto, lakini hata hivyo
hawakuelewa;
iliwateketeza, lakini hawakuyatia
moyoni.

*Mwokozi Pekee Wa Israeli*

43 [d]Lakini sasa hili ndilo asemalo
BWANA,
yeye aliyekuumba, ee Yakobo,
yeye aliyekuhuluku, ee Israeli:
"Usiogope kwa maana
nimekukomboa,
nimekuita wewe kwa jina lako,
wewe u wangu.
2 [e]Unapopita kwenye maji makuu,
nitakuwa pamoja nawe,
unapopita katika mito ya maji,
hayatakugharikisha.
Utakapopita katika moto,
hutaungua,
miali ya moto haitakuunguza.
3 [f]Kwa kuwa Mimi ndimi BWANA,
Mungu wako,
yeye Aliye Mtakatifu wa Israeli,
Mwokozi wako.
Ninaitoa Misri kuwa fidia yako,
Kushi na Seba badala yako.
4 [g]Kwa kuwa wewe ni wa thamani na
wa kuheshimiwa machoni
pangu,
nami kwa kuwa ninakupenda,
nitatoa watu badala yako
na mataifa badala ya maisha yako.
5 [h]Usiogope, kwa kuwa mimi nipo
pamoja nawe,
nitawaleta watoto wako kutoka
mashariki,
na kukukusanya kutoka
magharibi.
6 [i]Nitaiambia kaskazini, 'Watoe!'
nayo kusini, 'Usiwazuie.'
Walete wana wangu kutoka mbali,
na binti zangu kutoka miisho ya
dunia:
7 [j]kila mmoja ambaye ameitwa kwa
Jina langu,
niliyemuumba kwa utukufu
wangu,
niliyemhuluku na kumfanya."
8 [k]Uwaongoze wale wenye macho
lakini hawaoni,
wenye masikio lakini hawasikii.
9 [l]Mataifa yote yanakutanika pamoja,
na makabila yanakusanyika.

---

[a]**42:23** Kum 32:29; Za 81:13; Isa 47:7; 48:18; 57:11
[b]**42:24** 2Fal 17:6; Isa 43:28; 10:5-6
[c]**42:25** Hos 7:9; Nah 1:6; 2Fal 22:13; Ay 40:11; Eze 7:19; 2Fal 25:9; Isa 29:13
[d]**43:1** Mwa 2:7; 32:28; Isa 45:3-4; Kut 6:6; Isa 42:6; 27:11; Ay 19:25
[e]**43:2** Mwa 26:3; Kum 31:6-8; Isa 30:27; 8:7; Dan 3:25-27; Kut 14:22; Isa 29:6
[f]**43:3** Mit 21:18; Kut 30:2; Isa 20:3; Mwa 10:7; Eze 29:20; Za 68:31; Amu 2:18; Kut 14:30
[g]**43:4** Isa 63:9; Ufu 3:9; Kut 19:5-6; Isa 49:5
[h]**43:5** Isa 44:2; Mwa 21:22; Kut 14:22; Mdo 18:10; Yer 30:10-11; Mt 8:11; Zek 8:7; Isa 24:14
[i]**43:6** Eze 16:61; 2Kor 6:18; Eze 36:24; Yer 23:8; Kum 30:4; Isa 60:4; 11:12
[j]**43:7** Yak 2:7; Isa 29:23; Yer 15:16; Efe 2:10; Isa 56:5; 62:2; 63:19; Za 89:9
[k]**43:8** Isa 6:9-10; 42:20; Eze 12:2
[l]**43:9** Isa 45:20; 48:14; 41:26

Ni nani miongoni mwao
aliyetangulia kutuambia haya,
na kututangazia mambo
yaliyopita?
Walete mashahidi wao ili
kuwathibitisha kuwa
walikuwa sahihi,
ili wengine waweze kusikia,
waseme, “Ni kweli.”

10 [a]“Ninyi ni mashahidi wangu,” asema
Bwana,
“na mtumishi wangu
niliyemchagua,
ili mpate kunijua na kuniamini,
na kutambua kwamba Mimi ndiye.
Kabla yangu hakuna mungu
aliyefanyizwa,
wala hatakuwepo mwingine baada
yangu.
11 [b]Mimi, naam mimi, ndimi Bwana,
zaidi yangu hakuna mwokozi.
12 [c]Nimedhihirisha, kuokoa na
kutangaza:
Mimi, wala si mungu mgeni
katikati yenu.
Ninyi ni mashahidi wangu,” asema
Bwana,
“kwamba Mimi ndimi Mungu.
13 [d]Naam, tangu siku za kale, Mimi
ndiye.
Hakuna hata mmoja awezaye kuokoa
kutoka mkononi wangu.
Mimi ninapotenda,
ni nani awezaye kutangua?”

*Huruma Za Mungu, Na Kukosa Uaminifu Kwa Israeli*

14 [e]Hili ndilo Bwana asemalo,
Mkombozi wako, yeye Aliye
Mtakatifu wa Israeli:
“Kwa ajili yenu nitatumana Babeli
na kuwaleta Wakaldayo wote
kama wakimbizi,
katika meli walizozionea fahari.
15 [f]Mimi ndimi Bwana, yeye Aliye
Mtakatifu wako,
Muumba wa Israeli, Mfalme
wako.”

16 [g]Hili ndilo asemalo Bwana,
yeye aliyefanya njia baharini,
mahali pa kupita kwenye maji
mengi,
17 [h]aliyeyakokota magari ya vita na
farasi,
jeshi pamoja na askari wa msaada,
nao wakalala huko, wala
hawatainuka tena kamwe,
wakakomeshwa, na wakazimika
kama utambi:
18 [i]“Msiyakumbuke mambo yaliyopita,
wala msiyatafakari mambo ya
zamani.
19 [j]Tazama, nitafanya jambo jipya!
Sasa litachipuka, je,
hamtalitambua?
Nitafanya njia jangwani
na vijito vya maji katika nchi
kame.
20 [k]Wanyama wa mwituni
wataniheshimu,
mbweha na bundi,
kwa sababu ninawapatia maji
jangwani,
na vijito katika nchi kame,

[a] **43:10** Isa 41:8-9; 19:21; Za 86:10; Yer 14:22; Yos 24:22; Kum 4:35; Isa 45:5-6, 14
[b] **43:11** Isa 42:8; Za 18:31; Isa 25:9; 63:4; Kut 6:2
[c] **43:12** Kum 32:16; Za 81:9; Isa 44:8
[d] **43:13** Hes 23:8; Ay 9:12; Za 90:2; Mit 8:23; Kum 32:39; Isa 48:12
[e] **43:14** Isa 13:14-15; 23:13; Kut 15:13; Ay 19:25; Isa 41:20
[f] **43:15** Isa 42:8; 27:11; 45:11; 41:21
[g] **43:16** Kut 14:29; Za 77:19; Kut 15:8; Isa 11:15
[h] **43:17** Za 118:12; Kut 14:4-9, 22; Za 76:5-6; Ay 13:25; Yer 51:21; Eze 38:4
[i] **43:18** Isa 41:22
[j] **43:19** Hes 20:11; Yer 23:8-9; Ufu 21:5; Isa 40:3; 41:22; Yer 16:14-15; 2Kor 5:17; Isa 35:7
[k] **43:20** Hes 20:8; Isa 48:21; 41:17; Za 148:10; Isa 13:22

ili kuwapa watu wangu maji, wale
niliowachagua,
21 [a]watu wale niliowaumba kwa ajili
yangu,
ili wapate kutangaza sifa zangu.

22 "Hata hivyo hukuniita mimi, ee
Yakobo,
hujajitaabisha kwa ajili yangu, ee
Israeli.
23 [b]Hujaniletea kondoo kwa ajili ya
sadaka za kuteketezwa,
wala kuniheshimu kwa dhabihu
zako.
Sikukulemea kwa sadaka za nafaka
wala kukuchosha kwa kuhitaji
uvumba.
24 [c]Hukuninunulia uvumba wowote
wenye manukato,
wala hukunipa kwa ukarimu
mafuta ya wanyama wa dhabihu
zako.
Lakini umenilemea kwa dhambi
zako,
na kunitaabisha kwa makosa yako.

25 [d]"Mimi, naam mimi, ndimi nizifutaye
dhambi zako,
kwa ajili yangu mwenyewe,
wala sizikumbuki dhambi zako
tena.
26 [e]Tafakari mambo yaliyopita,
njoo na tuhojiane,
leta shauri lako uweze kupewa
haki yako.
27 [f]Baba yako wa kwanza alitenda
dhambi,
wasemaji wako wameasi dhidi
yangu.
28 [g]Kwa hiyo nitawaaibisha wakuu wa
Hekalu lako,
nami nitamtoa Yakobo
aangamizwe,
na Israeli adhihakiwe.

*Israeli Aliyechaguliwa*

44 [h]"Lakini sasa sikiliza, ee Yakobo,
mtumishi wangu,
Israeli, niliyemchagua.
2 [i]Hili ndilo asemalo BWANA,
yeye aliyekuhuluku, aliyekuumba
tumboni,
yeye atakayekusaidia:
Usiogope, ee Yakobo, mtumishi
wangu,
Yeshuruni,[j] niliyekuchagua.
3 [k]Kwa maana nitamimina maji juu ya
nchi yenye kiu,
na vijito vya maji juu ya ardhi
iliyokauka;
nitamimina Roho wangu juu ya
watoto wako,
nayo baraka yangu juu ya wazao
wako.
4 [l]Nao watachipua kama manyasi
katika shamba la majani,
kama mierezi kando ya vijito vya
maji yatiririkayo.
5 [m]Mmoja atasema, 'Mimi ni wa
BWANA';
mwingine atajiita kwa jina la
Yakobo;
vilevile mwingine ataandika juu ya
mkono wake, 'Wa BWANA,'
na kujiita kwa jina la Israeli.

---

[a]**43:21** Za 66:2; 1Pet 2:9; Mwa 2:7; Mal 3:17; Za 102:18
[b]**43:23** Zek 7:5-6; Kut 30:35; Yer 7:22; Amo 5:25; Kut 29:41; Mik 6:3; Mal 1:12-13
[c]**43:24** Kut 30:23; Mal 2:17; Isa 7:13; Yer 8:21; Law 3:9; Yer 44:22
[d]**43:25** 2Sam 12:13; Lk 5:21; Eze 20:44; Yer 31:34; Ay 7:21; 2Nya 6:21; Isa 64:9
[e]**43:26** Isa 1:18; 41:1; 49:25; 50:8
[f]**43:27** Rum 5:12; Isa 28:7; Yer 5:31; Mwa 12:18; Isa 9:15; 24:20
[g]**43:28** Eze 5:15; Za 39:8; Hes 5:27; Kum 13:15; Isa 42:24; Zek 5:3; Yer 24:9
[h]**44:1** Yer 30:10; Isa 41:8-10; Mwa 16:11; Isa 14:1
[i]**44:2** Hes 23:21; Kum 32:15; Za 149:2; 139:13; Isa 41:10; Yer 30:10; 46:27
[j]2 Yeshuruni hapa maana yake ni Yeye aliye mnyofu, yaani Israeli (ona pia Kum 32:15).
[k]**44:3** Yn 4:10; Yoe 3:18; Isa 65:23; Yoe 2:28; Yn 7:37-39; Mit 9:5; Eze 36:27
[l]**44:4** Law 23:40; Ay 40:22; 5:25; Za 72:16
[m]**44:5** Kut 13:9; Neh 9:38; Zek 13:9; 14:16; 8:20-22; Yer 50:5

*Ni Bwana, Siyo Sanamu*

6 [a]"Hili ndilo asemalo Bwana,
Mfalme wa Israeli na Mkombozi,
Bwana Mwenye Nguvu Zote:
Mimi ni wa kwanza na Mimi ni wa mwisho;
zaidi yangu hakuna Mungu.
7 [b]Ni nani basi aliye kama mimi? Yeye na atangaze.
Yeye atangaze na kuweka mbele yangu
ni kitu gani kilichotokea tangu nilipoumba watu wangu wa kale,
tena ni nini kitakachotokea:
naam, yeye na atoe unabii ni nini kitakachokuja.
8 [c]Msitetemeke, msiogope.
Je, sikutangaza hili, na kutoa unabii tangu zamani?
Ninyi ni mashahidi wangu.
Je, yuko Mungu zaidi yangu mimi?
Hasha, hakuna Mwamba mwingine;
mimi simjui mwingine."

9 [d]Wote wachongao sanamu ni ubatili,
navyo vitu wanavyovithamini havifai kitu.
Wale ambao wanazitetea ni vipofu,
ni wajinga, nao waaibika.
10 [e]Ni nani atengenezaye mungu na kusubu sanamu,
ambayo haiwezi kumfaidia kitu chochote?
11 [f]Yeye pamoja na wenziwe wa aina yake wataaibishwa,
mafundi wao si kitu ila ni wanadamu tu.
Wote wakusanyike pamoja na kuwa na msimamo wao,
watashushwa chini kwa hofu na kwa fedheha.

12 [g]Muhunzi huchukua kifaa
na kukifanyia kazi kwenye makaa ya moto,
hutengeneza sanamu kwa nyundo,
huifanyiza kwa nguvu za mkono wake.
Huona njaa na kupoteza nguvu zake,
asipokunywa maji huzimia.
13 [h]Seremala hupima kwa kutumia kamba
na huuchora mstari kwa kalamu;
huchonga kwa patasi
na kutia alama kwa bikari.
Huifanyiza katika umbo la binadamu,
la mwanadamu katika utukufu wake wote,
ili iweze kukaa katika sehemu yake ya ibada ya miungu.
14 [i]Hukata miti ya mierezi,
huchukua mtiriza au mwaloni.
Huuacha ukue miongoni mwa miti ya msituni,
au hupanda msunobari, nayo mvua huufanya ukue.
15 [j]Ni kuni ya binadamu:
yeye huchukua baadhi yake na kuota moto,
huwasha moto na kuoka mkate.
Lakini pia huutumia kumtengeneza mungu na akamwabudu,
huitengeneza sanamu na kuisujudia.
16 [k]Sehemu ya kuni huziweka motoni,
akapikia chakula chake,
hubanika nyama na kula hadi ashibe.
Huota moto na kusema,
"Aha! Ninahisi joto, ninaona moto."

---

[a]**44:6** Ay 19:25; Isa 41:4; Ufu 22:13; Isa 43:10; 1Nya 17:20
[b]**44:7** Kum 32:39; Isa 41:22-26
[c]**44:8** Isa 43:10; Mwa 49:24; Kum 4:35; Isa 42:9
[d]**44:9** Isa 41:24; Kum 4:28; Kut 20:4; Law 19:4; Isa 40:19; 1:29; Yer 22:22
[e]**44:10** Yer 10:5; Mdo 19:24; Isa 41:29
[f]**44:11** 2Fal 19:18; Isa 42:17; 37:19; 1:29
[g]**44:12** Isa 40:19; 54:16; Yer 10:3-5; Mdo 17:29; Isa 41:6-7; 40:28
[h]**44:13** Isa 41:7; Za 115:4-7; Amu 17:4-5
[i]**44:14** Isa 41; 19
[j]**44:15** Ufu 9:20; 2Nya 25:14
[k]**44:16** Isa 47:14

17 [a]Mabaki yake hutengeneza mungu,
sanamu yake;
yeye huisujudia na kuiabudu.
Huiomba na kusema,
"Niokoe; wewe ni mungu wangu."
18 [b]Hawajui chochote, hawaelewi
chochote,
macho yao yamefungwa hata
hawawezi kuona,
akili zao zimefungwa hata
hawawezi kufahamu.
19 [c]Hakuna anayefikiri,
hakuna mwenye maarifa wala
ufahamu wa kusema,
"Sehemu yake nilitumia kwa kuni;
hata pia nilioka mkate juu ya
makaa yake,
nikabanika nyama na kuila.
Je, nifanye machukizo kwa kile
kilichobaki?
Je, nisujudie gogo la mti?"
20 [d]Hujilisha kwa majivu, moyo
uliodanganyika humpotosha;
hawezi kujiokoa mwenyewe, au
kusema,
"Je, kitu hiki kilichoko katika
mkono wangu wa kuume si ni
uongo?"

21 [e]"Ee Yakobo, kumbuka mambo haya,
ee Israeli, kwa kuwa wewe ni
mtumishi wangu.
Nimekuumba wewe, wewe ni
mtumishi wangu.
Ee Israeli, sitakusahau.
22 [f]Nimeyafuta makosa yako kama
wingu,
dhambi zako kama ukungu wa
asubuhi.
Nirudie mimi,
kwa kuwa nimekukomboa wewe."

23 [g]Enyi mbingu, imbeni kwa furaha,
kwa maana BWANA amefanya
jambo hili.
Ee vilindi vya dunia, piga kelele.
Enyi milima, pazeni sauti kwa
nyimbo,
enyi misitu na miti yenu yote,
kwa maana BWANA amemkomboa
Yakobo,
ameuonyesha utukufu wake katika
Israeli.

*Yerusalemu Kukaliwa*

24 [h]"Hili ndilo asemalo BWANA,
Mkombozi wako, aliyekuumba
tumboni:

"Mimi ni BWANA,
niliyeumba vitu vyote,
niliyezitanda mbingu peke yangu,
niliyeitandaza nchi mwenyewe,

25 [i]"mimi huzipinga ishara za manabii
wa uongo,
na kuwatia upumbavu waaguzi,
niyapinduaye maarifa ya wenye
hekima,
na kuyafanya kuwa upuzi,
26 [j]niyathibitishaye maneno ya
watumishi wake,
na kutimiza utabiri wa wajumbe
wake,

"niambiaye Yerusalemu, 'Itakaliwa
na watu,'
niambiaye miji ya Yuda kuwa,
'Itajengwa,'
na kuhusu magofu yake, 'Mimi
nitayatengeneza,'
27 [k]niambiaye kilindi cha maji, 'Kauka,
nami nitakausha vijito vyako,'

---

[a]**44:17** 1Fal 18:26; Amu 10:14; Isa 47:15; Kut 20:5; Isa 45:20; 46:7
[b]**44:18** Isa 16:12; Yer 4:22; Isa 29:10; Rum 11:8-10; Isa 6:9-10; Yer 10:8, 14-15
[c]**44:19** Isa 45:20; Kum 27:15; Isa 5:13; 27:11; 40:20
[d]**44:20** Hos 4:12; Ay 15:31; 2Tim 3:13; Rum 1:25; Za 102; 9; 2The 2:11; Kum 4:28
[e]**44:21** Isa 46:8; Zek 10:9; Za 27:10; Yer 31:20; Isa 49:15; 27:11
[f]**44:22** 2Nya 6:21; Mdo 3:19; Mt 20:28; Mal 3:7; 2Sam 12:13; Ay 22:23; 1Kor 6:20
[g]**44:23** Za 98:4; Isa 42:10; Za 98:8; Yer 30:19; Isa 12:6; 1Nya 16:31; Za 65:13; Kut 16:7
[h]**44:24** Ay 19:25; Isa 43:15; 42:5; Za 139:13
[i]**44:25** Law 19:26; Ay 5:13; 2Sam 15:31; 1Kor 1:19-20, 27; Za 33:10; 1Sam 6:2; Isa 47:13
[j]**44:26** Zek 1:6; Isa 59:21; Mt 5:18; Ezr 9:9; Isa 46:10; Yer 23:20; 39:16
[k]**44:27** Isa 11:15; 19:5; Ufu 16:12

28 [a]nisemaye kuhusu Koreshi, 'Yeye ni
mchungaji wangu,
naye atatimiza yote
yanipendezayo;
atauambia Yerusalemu,
"Ukajengwe tena,"
na kuhusu Hekalu, "Misingi yake
na iwekwe." '

*Koreshi Chombo Cha Mungu*

45 [b]"Hili ndilo asemalo BWANA kwa
mpakwa mafuta wake,
Koreshi, ambaye nimemshika
mkono wake wa kuume
kutiisha mataifa mbele yake
na kuwavua wafalme silaha zao,
kufungua milango mbele yake
ili malango yasije yakafungwa:
2 [c]Nitakwenda mbele yako
na kusawazisha milima;
nitavunjavunja malango ya shaba
na kukatakata mapingo ya chuma.
3 [d]Nitakupa hazina za gizani,
mali zilizofichwa mahali pa siri,
ili upate kujua ya kwamba Mimi
ndimi BWANA,
Mungu wa Israeli, akuitaye kwa
jina lako.
4 [e]Kwa ajili ya Yakobo mtumishi
wangu,
Israeli niliyemchagua,
nimekuita wewe kwa jina lako,
na kukupa jina la heshima,
ingawa wewe hunitambui.
5 [f]Mimi ndimi BWANA, wala hakuna
mwingine,
zaidi yangu hakuna Mungu.
Nitakutia nguvu,
ingawa wewe hujanitambua,
6 [g]ili kutoka mawio ya jua
mpaka machweo yake,
watu wapate kujua kwamba hakuna
Mungu mwingine ila Mimi.
Mimi ndimi BWANA wala hakuna
mwingine.
7 [h]Mimi ninaumba nuru na kuhuluku
giza,
ninaleta mafanikio na kusababisha
maafa.
Mimi, BWANA, huyatenda haya
yote.

8 [i]"Enyi mbingu juu, nyesheni haki,
mawingu na yaidondoshe.
Dunia na ifunguke sana,
wokovu na uchipuke,
haki na ikue pamoja nao.
Mimi, BWANA, ndiye niliyeiumba.

9 [j]"Ole wake yeye ashindanaye na
Muumba wake,
yeye ambaye ni kigae tu kati ya
vigae juu ya ardhi.
Je, udongo wa kufinyangia
humwambia mfinyanzi,
'Unatengeneza nini wewe?'
Je, kazi yako husema,
'Hana mikono'?
10 Ole wake amwambiaye baba yake,
'Umezaa nini?'
Au kumwambia mama yake,
'Umezaa kitu gani?'

11 [k]"Hili ndilo asemalo BWANA,
yeye Aliye Mtakatifu wa Israeli na
Muumba wake:
Kuhusu mambo yatakayokuja,
je, unaniuliza habari za watoto
wangu,
au kunipa amri kuhusu kazi za
mikono yangu?

---

[a]**44:28** 2Nya 36:22-23; Ezr 1:2-4; Isa 14:32; 41:2; 28:16; 58:12
[b]**45:1** Za 73:23; Mik 4:13; Yer 50:20, 35; 51:20; Isa 48:14; 41:13; Za 45:7
[c]**45:2** Isa 40:4; Mao 2:9; Nah 3:13; Kut 23:20; Isa 13:2; Za 107:16; Yer 51:30
[d]**45:3** Kut 33:12; Isa 41:23; Yer 41:8; 2Fal 24:13; Yer 50:37; 51:13
[e]**45:4** Mdo 17:23; Isa 41:8-9; 14:1
[f]**45:5** Kum 32:12; Za 18:31, 39; Eze 30:24-25; Isa 44:8; 43:10
[g]**45:6** Za 113:3; Mal 1:11; Isa 14:13-14; Sef 2:15; Isa 43:5; 11:9
[h]**45:7** Mao 3:38; Amo 3:6; Kut 10:22; Isa 14:15; 31:2
[i]**45:8** Yoe 3:18; Hos 12:10; Mal 4:2; Za 85:9; 72:6; Isa 41:2; 46:13; Amu 5:24; Isa 60:21
[j]**45:9** Ay 27:2; Yer 18:16; 1Kor 10:22; Rum 9:20-21; Ay 12:13; 15:25; 33:13; 9:12
[k]**45:11** Yer 31:9; Za 8:6; Isa 19:25; Za 149:2; Isa 51:13

12 [a]Mimi ndiye niliyeumba dunia
na kumuumba mwanadamu juu yake.
Mikono yangu mwenyewe ndiyo iliyozitanda mbingu,
nikayapanga majeshi yake yote ya angani.
13 [b]Mimi nitamwinua Koreshi katika haki yangu:
nitazinyoosha njia zake zote.
Yeye atajenga mji wangu upya,
na kuwaweka huru watu wangu walio uhamishoni,
lakini si kwa kulipiwa fedha wala kupewa zawadi,
asema Bwana Mwenye Nguvu Zote."

14 [c]Hili ndilo asemalo Bwana:

"Mazao ya Misri na bidhaa za Kushi,
nao wale Waseba warefu,
watakujia na kuwa wako,
watakujia wakijikokota nyuma yako,
watakujia wamefungwa minyororo.
Watasujudu mbele yako
wakikusihi na kusema,
'Hakika Mungu yu pamoja nawe,
wala hakuna mwingine;
hakuna Mungu mwingine.' "

15 [d]Hakika wewe u Mungu unayejificha,
Ee Mungu na Mwokozi wa Israeli.
16 [e]Wote watengenezao sanamu wataaibika na kutahayarika;
wataenda kutahayarika pamoja.
17 [f]Lakini Israeli ataokolewa na Bwana
kwa wokovu wa milele;
kamwe hutaaibika wala kutatahayarika,
milele yote.

18 [g]Kwa kuwa hili ndilo asemalo Bwana,
yeye aliyeumba mbingu,
ndiye Mungu;
yeye aliyeifanya dunia na kuiumba,
yeye ndiye aliiwekea misingi imara,
hakuiumba ili iwe tupu,
bali aliiumba ikaliwe na viumbe vyake.
Anasema:
"Mimi ndimi Bwana,
wala hakuna mwingine.
19 [h]Sijasema sirini,
kutoka mahali fulani katika nchi ya giza;
sijawaambia wazao wa Yakobo,
'Nitafuteni bure.'
Mimi, Bwana, nasema kweli;
ninatangaza lililo sahihi.

20 [i]"Kusanyikeni pamoja mje,
enyi wakimbizi kutoka mataifa.
Wale wabebao sanamu za mti ni watu wasio na akili,
wale waombao miungu isiyoweza kuokoa.
21 [j]Tangazeni litakalokuwepo, lisemeni hilo,
wao na wafanye shauri pamoja.
Ni nani aliyetangulia kusema hili tangu zamani,
aliyetangaza tangu zamani za kale?
Je, haikuwa Mimi, Bwana?
Wala hapana Mungu mwingine zaidi yangu mimi,
Mungu mwenye haki na Mwokozi;
hapana mwingine ila mimi.

---

[a]**45:12** Isa 42:5; Yer 27:5; Neh 9:6; Ay 38:32; Isa 48:13
[b]**45:13** Rum 3:24; Isa 52:3; 2Nya 36:22; Isa 41:2; 1Fal 8:36; Za 26:12
[c]**45:14** 2Sam 3:34; Isa 14:2; Zek 8:20-23; 2Sam 8:2; Isa 18:7; Mwa 27:29; Yer 16:19; 1Kor 14:25; Isa 43:10
[d]**45:15** Kum 31:17; Isa 8:17; Za 44:24; Isa 25:9; 1:15
[e]**45:16** Za 35:4; Isa 1:29
[f]**45:17** Yer 23:6; Rum 11:26; Isa 26:4; Yer 33:16; Isa 12:2; Mwa 30:23; Isa 29:22
[g]**45:18** Mwa 1:2, 26; Isa 42:5; Kum 4:25
[h]**45:19** Neh 9:13; Isa 48:16; 65:4, 9; Yer 31:36; Kum 30:11; Yer 2:31; Kum 4:49
[i]**45:20** Yer 2:28; Isa 43:9; 44:19; Rum 1:22; Kum 32:37; Yer 10:5; Za 115:7
[j]**45:21** Za 46:10; Mk 12:32; Isa 41:22; 46:10; 25:9; Za 11:7

22 [a]“Nigeukieni mimi, nanyi
mkaokolewe,
enyi miisho yote ya dunia;
kwa maana mimi ndimi Mungu,
wala hapana mwingine.
23 [b]Nimeapa kwa nafsi yangu,
kinywa changu kimenena katika
uadilifu wote
neno ambalo halitatanguka:
Kila goti litapigwa mbele zangu,
kwangu mimi kila ulimi utaapa.
24 [c]Watasema kuhusu mimi,
‘Katika BWANA peke yake
ndiko kuna haki na nguvu.’ ”
Wote ambao wamemkasirikia Mungu
watamjia yeye, nao
watatahayarika.
25 [d]Lakini katika BWANA wazao wote
wa Israeli
wataonekana wenye haki na
watashangilia.

*Miungu Ya Babeli*

46 [e]Beli anasujudu hadi nchi, Nebo
anainama;
sanamu zao zabebwa na wanyama
wa mizigo.
Vinyago hivi mnavyobeba kila
mahali ni mzigo wa kulemea,
mzigo kwa waliochoka.
2 [f]Vinyago pamoja na wale
wanaovibeba wanainama
chini;
hiyo miungu haiwezi kuwaokoa
watu,
wote wanakwenda utumwani
pamoja.

3 [g]“Nisikilizeni mimi, ee nyumba ya
Yakobo,
ninyi nyote mliobaki wa nyumba
ya Israeli,
ninyi ambao nimewategemeza tangu
mlipotungwa mimba,
nami nimewabeba tangu kuzaliwa
kwenu.
4 [h]Hata mpaka wakati wa uzee wenu
na mvi, Mimi ndiye,
Mimi ndiye nitakayewasaidia
ninyi.
Nimewahuluku, nami nitawabeba,
nitawasaidia ninyi na kuwaokoa.

5 [i]“Mtanilinganisha na nani, au
mtanihesabu kuwa sawa na
nani?
Ni nani mtakayenifananisha naye
ili tuweze kulinganishwa?
6 [j]Wengine humwaga dhahabu kutoka
kwenye mifuko yao,
na kupima fedha kwenye mizani;
huajiri mfua dhahabu kutengeneza
mungu,
kisha huisujudia na kuiabudu.
7 [k]Huiinua mabegani na kuichukua;
huiweka mahali pake, papo hapo
ndipo isimamapo.
Wala haiwezi kusogea kutoka
mahali pale.
Ingawa mtu huililia, haimjibu;
haiwezi kumwokoa kwenye taabu
zake.

8 [l]“Kumbukeni hili, litieni akilini,
liwekeni moyoni, enyi waasi.
9 [m]Kumbukeni mambo yaliyopita, yale
ya zamani za kale;
mimi ndimi Mungu, wala hakuna
mwingine;

[a]**45:22** Zek 12:10; Hes 21:8-9; Mwa 49:10; Isa 11:9-12; 44:22; 2Nya 20:12
[b]**45:23** Mwa 22:16; Ebr 6:13; Flp 2:10-11; Isa 14:24; Za 63:11; Kum 6:13
[c]**45:24** Yer 33:16; Isa 41:11; Kum 33:29; Isa 40:26
[d]**45:25** Isa 24:23; 41:16; 49:4
[e]**46:1** Yer 51:44; Isa 45:20; 21:9; Yer 50:2
[f]**46:2** 2Sam 5:21; Yer 51:47; Amu 18:17-18
[g]**46:3** Isa 48:12; Kut 19:14; Isa 44:2; Kum 1:31; Za 28:9; 22:10
[h]**46:4** Mal 3:6; Za 71:18; Isa 43:13; Kum 32:39; Za 18:35; 119:117
[i]**46:5** Kut 15:11; Ay 41:10; Isa 40:18, 25; Yer 49:19
[j]**46:6** Kut 20:5; Hos 13:2; Isa 40:19; 44:17
[k]**46:7** 1Sam 5:3; Isa 41:7; 1Fal 16:26
[l]**46:8** Isa 44:21; 1:2
[m]**46:9** Kum 8:10; Kut 8:10; Mk 12:32; Isa 41:22; 45:21

mimi ndimi Mungu,
wala hakuna mwingine aliye kama mimi.
10 [a]Ni mimi nitangazaye mwisho tangu mwanzo,
naam, tangu zamani za kale,
mambo ambayo hayajatendeka.
Ninasema: Kusudi langu ndilo litakalosimama,
nami nitatenda mapenzi yangu yote.
11 [b]Kutoka mashariki ninaita ndege awindaye;
kutoka nchi ya mbali,
mtu atakayetimiza kusudi langu.
Lile ambalo nimelisema, ndilo nitakalolitimiza;
lile nililolipanga, ndilo nitakalolitenda.
12 [c]Nisikilizeni, ninyi wenye mioyo migumu,
ninyi mlio mbali na haki.
13 [d]Ninaleta haki yangu karibu,
haiko mbali;
wala wokovu wangu hautachelewa.
Nitawapa Sayuni wokovu,
Israeli utukufu wangu.

*Anguko La Babeli*

47 [e]"Shuka uketi mavumbini,
ee Bikira Binti Babeli;
keti chini pasipo na kiti cha enzi,
ee binti wa Wakaldayo.
Hutaitwa tena mwororo wala wa kupendeza.
2 [f]Chukua mawe ya kusagia, usage unga,
vua shela yako.
Pandisha mavazi yako, ondoa viatu vyako,
vuka vijito kwa shida.
3 [g]Uchi wako utafunuliwa
na aibu yako itaonekana.
Nitalipa kisasi;
sitamhurumia hata mmoja."

4 [h]Mkombozi wetu: BWANA Mwenye Nguvu Zote ndilo jina lake;
ndiye yeye Aliye Mtakatifu wa Israeli.

5 [i]"Keti kimya, ingia gizani,
Binti wa Wakaldayo,
hutaitwa tena malkia wa falme.
6 [j]Niliwakasirikia watu wangu
na kuaibisha urithi wangu;
niliwatia mikononi mwako,
nawe hukuwaonea huruma.
Hata juu ya wazee
uliweka nira nzito sana.
7 [k]Ukasema, 'Nitaendelea
kuwa malkia milele!'
Lakini hukutafakari mambo haya
wala hukuwaza juu ya kile kingeweza kutokea.

8 [l]"Sasa basi, sikiliza, ewe kiumbe mpenda anasa,
ukaaye mahali pako pa salama,
na kujiambia mwenyewe,
'Mimi ndiye, wala hakuna mwingine zaidi yangu.

[a]**46:10** Mit 19:21; Efe 1:11; Mdo 5:39; Isa 45:21; 41:22; 7:7-9; 44:26
[b]**46:11** Mwa 41:25; Yer 44:28; Amu 4:10; Ezr 1:2; Isa 8:5
[c]**46:12** Yer 2:5; Za 119:150; Rum 10:3; Kut 32:9; Isa 9:9
[d]**46:13** Isa 24:23; Mdo 13:36; Rum 1:17; Isa 1:26; 45:8; Rum 3:21; Yoe 2:32
[e]**47:1** Mao 2:10; Isa 21:9; 23:12; Yer 51:33; Zek 2:7; Ay 2:13; Isa 29:4
[f]**47:2** Mt 24:41; Kut 11:5; Amu 16:21; Mwa 24:65; Isa 32:11
[g]**47:3** Mwa 2:25; Rum 12:19; Neh 3:5; Isa 13:18-19; 20:4; 34:8; Eze 16:37
[h]**47:4** Yer 50:34; Amo 4:13; Isa 48:2, 17; Ay 19:25
[i]**47:5** Dan 2:37; Isa 13:10, 19; 9:2; 21:9; Ufu 17:18; Ay 2:13; Ufu 18:7
[j]**47:6** 2Nya 28:9; Isa 10:13; Zek 1:15; Kum 13:15; Yer 50:11; Isa 14:6; 42:24
[k]**47:7** Ufu 18:7; Kum 32:29; Isa 10:13; Dan 4:30; Isa 42:23-25
[l]**47:8** Isa 32:9; 45:6; 49:21; 54:4; Sef 2:15; Ufu 18:7

Kamwe sitakuwa mjane,
wala sitafiwa na watoto.'
9 [a]Haya mawili yatakupata, kufumba na kufumbua,
katika siku moja:
kufiwa na watoto, na ujane.
Yote yatakupata kwa kipimo kikamilifu,
ijapokuwa uchawi wako ni mwingi,
na uaguzi wako ni mwingi.
10 [b]Umeutegemea uovu wako,
nawe umesema, 'Hakuna yeyote anionaye.'
Hekima yako na maarifa yako vinakupoteza
unapojiambia mwenyewe,
'Mimi ndiye, wala hakuna mwingine zaidi yangu.'
11 [c]Maafa yatakujia,
nawe hutaweza kuyaondoa kwa uaguzi.
Janga litakuangukia,
wala hutaweza kulikinga kwa fidia;
msiba mkuu usioweza kuutabiri
utakujia ghafula.

12 [d]"Endelea basi na uaguzi wako,
na wingi wa uchawi wako,
ambao umeutumikia tangu utoto wako.
Labda utafanikiwa,
labda unaweza ukasababisha hofu kuu.
13 [e]Ushauri wote uliopokea umekuchosha bure!
Wanajimu wako na waje mbele,
wale watazama nyota watabiriao mwezi baada ya mwezi,
wao na wawaokoe na lile linalokuja juu yenu.
14 [f]Hakika wako kama mabua makavu;
moto utawateketeza.
Hawawezi hata kujiokoa wao wenyewe
kutokana na nguvu za mwali wa moto.
Hapa hakuna makaa ya kumtia mtu yeyote joto;
hapa hakuna moto wa kuota.
15 [g]Hayo ndiyo yote wanayoweza kuwatendea ninyi,
hawa ambao umetaabika nao
na kufanya nao biashara tangu utoto.
Kila mmoja atatoroka;
hakuna yeyote awezaye kukuokoa.

*Israeli Mkaidi*

48 [h]"Sikilizeni hili, ee nyumba ya Yakobo,
ninyi mnaoitwa kwa jina la Israeli,
na mnaotoka katika ukoo wa Yuda,
ninyi mnaoapa kwa jina la BWANA,
mnaomwomba Mungu wa Israeli,
lakini si katika kweli au kwa haki;
2 [i]ninyi mnaojiita raiya wa mji mtakatifu,
na kumtegemea Mungu wa Israeli,
BWANA Mwenye Nguvu Zote ndilo jina lake:
3 [j]Nilitoa unabii mambo ya kwanza tangu zamani,
kinywa changu kiliyatangaza na kuyafanya yajulikane;
kisha ghafula nikayatenda, nayo yakatokea.

---

[a]**47:9** 1The 5:3; Isa 13:8; Nah 3:4; Za 55:15; Mal 3:5; Kum 18:10-11; Ufu 9:21; 18:8-10
[b]**47:10** Ay 15:31; 2Fal 21:16; Isa 5:21; 29:15; Za 52:7; 62:10
[c]**47:11** Dan 5:30; Za 55:15; 1The 5:3; Isa 10:3; 14:15; 21:9; Lk 17:27; Isa 17:14
[d]**47:12** Kut 7:11
[e]**47:13** Yer 51:58; Hab 2:13; Isa 19:3; 5:29; 43:13; 57:10; 46:7; Dan 2:2
[f]**47:14** Isa 5:24; Nah 1:10; Yer 50:30-32; Isa 30:30; 10:17
[g]**47:15** Ufu 18:11; Isa 44:17
[h]**48:1** Kum 6:13; Kut 23:13; Dan 8:12; Zek 8:3; Mwa 17:5; 29:35; Isa 19:18
[i]**48:2** Neh 11:1; Rum 2:17; Mik 3:11; Isa 1:26; Mt 4:5; Isa 10:20; 47:4
[j]**48:3** Isa 40:21; 45:21; Yos 21:45; Isa 41:22; 17:14; 30:13

4 [a]Kwa kuwa nalijua jinsi ulivyokuwa mkaidi;
mishipa ya shingo yako ilikuwa chuma,
kipaji chako cha uso kilikuwa shaba.
5 [b]Kwa hiyo nilikuambia mambo haya tangu zamani,
kabla hayajatokea nilikutangazia
ili usije ukasema,
'Sanamu zangu zilifanya hayo;
kinyago changu cha mti na mungu wangu wa chuma aliyaamuru.'
6 [c]Umesikia mambo haya; yaangalie hayo yote.
Je, hutayakubali?

"Kuanzia sasa na kuendelea nitakueleza mambo mapya,
juu ya mambo yaliyofichika usiyoyajua.
7 [d]Yameumbwa sasa, wala si tangu zamani;
hukupata kuyasikia kabla ya siku ya leo.
Hivyo huwezi kusema,
'Naam, niliyajua hayo.'
8 [e]Hujayasikia wala kuyaelewa,
tangu zamani sikio lako halikufunguka.
Ninafahamu vyema jinsi ulivyo mdanganyifu,
uliitwa mwasi tangu kuzaliwa kwako.
9 [f]Kwa ajili ya Jina langu mwenyewe
ninaicheleweshа ghadhabu yangu,
kwa ajili ya sifa zangu nimeizuia isikupate,
ili nisije nikakukatilia mbali.
10 [g]Tazama, nimekusafisha, ingawa si kama fedha,
nimekujaribu katika tanuru ya mateso.
11 [h]Kwa ajili yangu mwenyewe,
kwa ajili yangu mwenyewe, nafanya hili.
Jinsi gani niliache Jina langu lichafuliwe?
Sitautoa utukufu wangu kwa mwingine.

*Israeli Anawekwa Huru*

12 [i]"Ee Yakobo, nisikilize mimi,
Israeli, ambaye nimekuita:
Mimi ndiye;
mimi ndimi mwanzo na mwisho.
13 [j]Mkono wangu mwenyewe uliweka misingi ya dunia,
nao mkono wangu wa kuume umezitanda mbingu;
niziitapo, zote husimama pamoja.

14 [k]"Kusanyikeni, ninyi nyote, msikilize:
Ni ipi miongoni mwa hizo sanamu
ambayo imetabiri vitu hivi?
Watu wa BWANA waliochaguliwa na kuungana
watatimiza kusudi lake dhidi ya Babeli;
mkono wa Mungu utakuwa dhidi ya Wakaldayo.
15 [l]Mimi, naam, Mimi, nimenena;
naam, nimemwita yeye.
Nitamleta,
naye atafanikiwa katika lile nililomtuma.

16 [m]"Nikaribieni na msikilize hili:

---

[a]**48:4** Kum 9:27; 31:27; Mdo 5:21; Isa 9:9; Kut 32:9; Eze 3:9; Mdo 7:51
[b]**48:5** Yer 44:15-18; Isa 42:9; 40:21
[c]**48:6** Isa 41:22; Rum 16:25
[d]**48:7** Isa 65:18; 45:21; Kut 6:7
[e]**48:8** Za 58:3; Kum 9:24; Isa 41:24; Mal 2:11-14; Isa 43:27
[f]**48:9** Yos 7:9; Ay 9:13; Za 78:38; 1Sam 12:22; Isa 37:35; 30:18
[g]**48:10** Za 66:10
[h]**48:11** 1Sam 12:22; Law 18:21; Isa 42:8; Kum 32:26-27; Eze 20:9; Yer 14:7, 21
[i]**48:12** Isa 46:3; 41:4; Ufu 22:13; Isa 43:13; 42:6
[j]**48:13** Ebr 1:10-12; Ay 9:8; Isa 34:16; 40:26; Kut 20:11; Isa 45:18
[k]**48:14** Isa 43:9; 46:10-11; 41:2, 22; Yer 50:45; Isa 21:9
[l]**48:15** Amu 4:10; Isa 45:1
[m]**48:16** Isa 45:19; Zek 2:8-11; Isa 33:13; 50:5-9; 11:2

"Tangu tangazo la kwanza sikusema
kwa siri;
wakati litokeapo, nitakuwako
hapo."

Sasa Bwana Mwenyezi amenituma,
kwa Roho wake.

[17] [a]Hili ndilo asemalo Bwana,
Mkombozi wako, yeye Aliye
Mtakatifu wa Israeli:
"Mimi ni Bwana, Mungu wako,
nikufundishaye ili upate faida,
nikuongozaye katika njia
ikupasayo kuiendea.
[18] [b]Laiti ungesikiliza kwa makini
maagizo yangu,
amani yako ingekuwa kama mto,
haki yako kama mawimbi ya
bahari.
[19] [c]Wazao wako wangekuwa kama
mchanga,
watoto wako kama chembe zake
zisizohesabika;
kamwe jina lao lisingefutiliwa mbali,
wala kuangamizwa kutoka mbele
zangu."

[20] [d]Tokeni huko Babeli,
kimbieni kutoka kwa Wakaldayo!
Tangazeni hili kwa kelele za
shangwe
na kulihubiri.
Lipelekeni mpaka miisho ya dunia;
semeni, "Bwana amemkomboa
mtumishi wake Yakobo."
[21] [e]Hawakuona kiu alipowaongoza
kupita jangwani;
alifanya maji yatiririke kutoka
kwenye mwamba kwa ajili
yao;
akapasua mwamba
na maji yakatoka kwa nguvu.

[22] [f]"Hakuna amani kwa waovu," asema
Bwana.

*Mtumishi Wa Bwana*

49 [g]Nisikilizeni, enyi visiwa, sikieni
hili,
ninyi mataifa mlio mbali:
Kabla sijazaliwa, Bwana aliniita,
tangu kuzaliwa kwangu, amelitaja
jina langu.
[2] [h]Akafanya kinywa changu kuwa
kama upanga ulionolewa,
katika uvuli wa mkono wake
akanificha;
akanifanya kuwa mshale
uliosuguliwa,
na kunificha katika podo lake.
[3] [i]Akaniambia, "Wewe u mtumishi
wangu,
Israeli, ambaye katika yeye
nitaonyesha utukufu wangu."
[4] [j]Lakini nilisema, "Nimetumika bure,
nimetumia nguvu zangu bure bila
faida.
Hata hivyo linalonistahili liko
mkononi mwa Bwana,
nao ujira wangu uko kwa Mungu
wangu."

[5] [k]Sasa Bwana asema:
yeye aliyeniumba tumboni kuwa
mtumishi wake,
kumrudisha tena Yakobo kwake
na kumkusanyia Israeli,
kwa maana nimepata heshima
machoni pa Bwana,
naye Mungu wangu amekuwa
nguvu yangu;

---

[a]**48:17** Ay 19:25; Za 32:4; Isa 54:8; 47:4; 28:9; Yer 7:13; Isa 49:10
[b]**48:18** Kum 5:29; Isa 42:23; Za 147:14; 45:8; Isa 54:13; 33:21; 45:5
[c]**48:19** Mwa 22:17; Ay 5:25; Yer 35:19; Isa 43:5; 61:9; Mwa 12:2; Isa 56:5
[d]**48:20** Zek 2:6-7; Ufu 18:4; Isa 12:6; Mik 4:10; Isa 52:11; Yer 48:6; 50:8
[e]**48:21** Isa 41:17; 33:16; 30:25; Kut 17:6; Za 105:41; Hes 20:11
[f]**48:22** Isa 3:11; 57:21; Ay 3:26
[g]**49:1** Isa 44:24; Yer 1:5; Lk 1:15; Isa 33:13; 11:11; Mt 1:20; Isa 7:14; 9:6; Kut 33:12
[h]**49:2** Za 64:3; Hos 6:5; Efe 6:17; Ay 40:18; Ufu 1:16; Kut 33:22; Zek 9:13
[i]**49:3** Isa 20:3; Zek 3:8; Law 10:3; Isa 44:23
[j]**49:4** Eze 3:19; Law 26:20; Isa 35:4; Ay 27:2; Isa 55:2; 65:23; 45:25; 54:17
[k]**49:5** Kum 30:4; Isa 11:12; 43:4; Za 139:13; Gal 1:15; Za 18:1

6 [a]yeye asema:
"Je, ni jambo dogo sana wewe kuwa mtumishi wangu
ili kurejeza makabila ya Yakobo,
na kuwarudisha wale Waisraeli niliowahifadhi?
Pia nitakufanya uwe nuru kwa ajili ya watu wa Mataifa,
ili upate kuleta wokovu wangu hata miisho ya dunia."

7 [b]Hili ndilo asemalo BWANA,
yeye Mkombozi na Aliye Mtakatifu wa Israeli,
kwake yeye aliyedharauliwa na kuchukiwa na taifa,
kwa mtumishi wa watawala:
"Wafalme watakuona na kusimama,
wakuu wataona na kuanguka kifudifudi,
kwa sababu ya BWANA, aliye mwaminifu,
yeye Aliye Mtakatifu wa Israeli, aliyekuchagua wewe."

*Kurejezwa Kwa Israeli*

8 [cd]Hili ndilo asemalo BWANA:

"Wakati wangu uliokubalika nitakujibu,
nami katika siku ya wokovu nitakusaidia;
nitakuhifadhi, nami nitakufanya
kuwa agano kwa ajili ya watu,
ili kurudisha nchi
na kugawanyia urithi tena wale waliokuwa ukiwa,
9 [e]kuwaambia mateka, 'Tokeni nje,'
nao wale walio gizani, 'Kuweni huru!'
"Watajilisha kando ya barabara
na kupata malisho yao juu ya kila kilima kilicho kitupu.
10 [f]Hawataona njaa wala kuona kiu,
wala hari ya jangwani au jua halitawapiga.
Yeye mwenye huruma juu yao atawaonyesha njia,
na kuwaongoza kando ya chemchemi za maji.
11 [g]Nitaifanya milima yangu yote kuwa barabara,
na njia kuu zangu zitainuliwa.
12 [h]Tazama, watakuja kutoka mbali:
wengine kutoka kaskazini,
wengine kutoka magharibi,
wengine kutoka nchi ya Sinimu."[i]

13 [j]Pigeni kelele kwa furaha, enyi mbingu;
furahi, ee dunia;
pazeni sauti kwa kuimba, enyi milima!
Kwa maana BWANA anawafariji watu wake,
naye atakuwa na huruma kwa watu wake walioumizwa.

14 [k]Lakini Sayuni alisema, "BWANA ameniacha,
Bwana amenisahau."

15 [l]"Je, mama aweza kumsahau mtoto
aliyeko matitini mwake akinyonya,
wala asiwe na huruma
juu ya mtoto aliyemzaa?
Ingawa anaweza kusahau,
mimi sitakusahau wewe!

[a]**49:6** Zek 8:22; Lk 2:32; Yn 11:52; Isa 9:2; Yon 1:9; Isa 26:18; Kum 30:4; Mdo 13:47
[b]**49:7** Isa 48:17; Za 69:7-9; Isa 52:15; Mwa 27:29; Za 22:6, 29; 86:9; Kum 7:9
[c]**49:8** Za 69:13; 2Kor 6:2; Law 25:10; Za 37:9; Isa 60:10; 41:10; 26:3; 5:2
[d]**49:8** Isa 44:28; Neh 2:17
[e]**49:9** Lk 4:19; Isa 41:18; Zek 9:12; Isa 42:7; Za 107:10
[f]**49:10** Isa 33:16; Ufu 7:16; Isa 35:7; Za 21:6; Isa 42:16; 33:21
[g]**49:11** Isa 11:6; Yer 31:9; Isa 40:4
[h]**49:12** Isa 2:3; 43:5-6; 59:19; Mt 8:11
[i]12 Sinimu hapa ina maana ya Aswani.
[j]**49:13** Za 98:4; 71:21; 2Kor 1:4; Isa 48:20; Za 96:11; 65:12-13; 9:12
[k]**49:14** Isa 40:9; Za 9:10; Isa 27:8; Za 71:11
[l]**49:15** Mt 7:11; Isa 44:21; 1Fal 3:26; Isa 66:13

16 [a]Tazama, nimekuchora kama muhuri
katika vitanga vya mikono yangu,
kuta zako zi mbele yangu daima.
17 [b]Wana wako wanaharakisha kurudi,
nao wale waliokuteka
wanaondoka kwako.
18 [c]Inua macho yako ukatazame pande
zote:
wana wako wote wanakusanyika
na kukujia.
Kwa hakika kama vile niishivyo,
utawavaa wote kama mapambo,
na kujifunga nao kama bibi arusi,"
asema BWANA.

19 [d]"Ingawa uliangamizwa na kufanywa
ukiwa,
na nchi yako ikaharibiwa,
sasa nafasi itakuwa finyu kwa ajili
ya watu wako,
nao wale waliokuangamiza
watakuwa mbali sana.
20 [e]Watoto waliozaliwa wakati wa
msiba wako
bado watakuambia,
'Mahali hapa ni finyu sana kwetu,
tupe eneo kubwa zaidi la kuishi.'
21 [f]Ndipo utasema moyoni mwako,
'Ni nani aliyenizalia hawa?
Nilikuwa nimefiwa, tena tasa;
nilikuwa nimehamishwa na
kukataliwa.
Ni nani aliyewalea hawa?
Niliachwa peke yangu,
lakini hawa wametoka wapi?' "

22 [g]Hili ndilo asemalo BWANA Mwenyezi:

"Tazama, nitawaashiria watu wa
Mataifa,
nitainua bendera yangu kwa
mataifa;
watawaleta wana wako mikononi
yao,
na kuwabeba binti zenu juu ya
mabega yao.
23 Wafalme watakuwa baba zenu wa
kuwalea,
na malkia wao watakuwa mama
zenu wa kuwalea.
Watasujudu mbele yako nyuso zao
zikigusa ardhi;
wataramba mavumbi yaliyo
miguuni mwako.
Ndipo utajua ya kuwa Mimi ndimi
BWANA;
wale wanaonitumaini mimi
hawataaibika."

24 [h]Je, nyara zaweza kuchukuliwa
kutoka kwa mashujaa wa vita,
au mateka kuokolewa kutoka kwa
watu wakali?

25 [i]Lakini hili ndilo asemalo BWANA:

"Naam, mateka watachukuliwa
kutoka kwa mashujaa,
na nyara zitapokonywa kutoka
kwa watu wakali.
Nitashindana na wale
wanaoshindana nawe,
nami nitawaokoa watoto wako.
26 [j]Nitawafanya wale wanaokuonea
kula nyama yao wenyewe,
watalewa kwa damu yao
wenyewe,
kama vile kwa mvinyo.
Ndipo wanadamu wote watajua
ya kuwa Mimi, BWANA, ni
Mwokozi wako,
Mkombozi wako, niliye Mwenye
Nguvu wa Yakobo."

---

[a]**49:16** Wim 8:6; Kut 28:9; Za 48:12-13; Isa 62:6; Mwa 38:18
[b]**49:17** Isa 49:19
[c]**49:18** Mit 17:6; Rum 14:11; Hes 14:21; Yer 2:32; Isa 11:12; 43:5; 54:9; 45:23
[d]**49:19** Law 26:33; Isa 62:4; Zek 10:10; Eze 36:10-11; Zek 2:4; Isa 60:18; 1:20
[e]**49:20** Mt 3:9; Rum 11:11, 12
[f]**49:21** Isa 5:13; Lk 15:5; Isa 60:4; 29:23; 66:7-8; 47:8; Yer 10:20; Mwa 15:2
[g]**49:22** Isa 60:10-11; Hes 11:12; Mwa 3:14; Za 72:9; Kut 6:2; Mik 7:17; Mwa 3:14
[h]**49:24** Mt 12:29; Mk 3:27; Lk 11:21
[i]**49:25** Yer 50:33-34; Isa 14:2; 25:9; Mk 3:27; Isa 13:11; 25:4-9; 1Sam 24:15
[j]**49:26** Isa 9:4, 20; Nah 1:10; Ufu 16:6; Eze 39:7; Hes 23:24; Yer 25:27; Isa 11:9; Ay 19:25; Isa 48:17; Mwa 49:24; Za 132:2

*Dhambi Ya Israeli Na Utii Wa Mtumishi*

50 [a]Hili ndilo asemalo BWANA:

"Iko wapi hati ya
talaka ya mama yako
ambayo kwayo niliachana naye?
Au nimewauza ninyi kwa nani
miongoni mwa watu wanaonidai?
Kwa ajili ya dhambi zenu mliuzwa,
kwa sababu ya makosa, mama
yenu aliachwa.
2 [b]Nilipokuja, kwa nini hakuwepo hata
mmoja?
Nilipoita, kwa nini hakuwepo hata
mmoja wa kujibu?
Je, mkono wangu ni mfupi mno hata
nisiweze kuwakomboa?
Je, mimi sina nguvu za kukuokoa?
Kwa kukemea tu naikausha bahari,
naigeuza mito ya maji kuwa
jangwa;
samaki wake wanaoza kwa kukosa
maji
na kufa kwa ajili ya kiu.
3 [c]Ninalivika anga weusi na kufanya
nguo ya gunia
kuwa kifuniko chake."

4 [d]BWANA Mwenyezi amenipa ulimi
uliofundishwa,
ili kujua neno limtegemezalo
aliyechoka.
Huniamsha asubuhi kwa asubuhi,
huamsha sikio langu lisikie kama
mtu afundishwaye.
5 [e]BWANA Mwenyezi amezibua
masikio yangu,
nami sikuwa mwasi,
wala sikurudi nyuma.
6 [f]Niliwapa mgongo wangu wale
wanipigao,
mashavu yangu wale wang'oao
ndevu zangu;
sikuuficha uso wangu kutokana na
fedheha
na kutemewa mate.
7 [g]Kwa sababu BWANA Mwenyezi
ananisaidia,
sitatahayarika.
Kwa hiyo nimekaza uso wangu kama
jiwe la gumegume,
nami ninajua sitaaibika.
8 [h]Yeye anipatiaye haki yangu yu
karibu.
Ni nani basi atakayeleta mashtaka
dhidi yangu?
Tukabiliane uso kwa uso!
Mshtaki wangu ni nani?
Ni nani aliye mshtaki wangu?
9 [i]Ni BWANA Mwenyezi anisaidiaye
mimi.
Ni nani huyo atakayenihukumu?
Wote watachakaa kama vazi,
nondo watawala wawamalize.

10 [j]Ni nani miongoni mwenu amchaye
BWANA,
na kulitii neno la mtumishi wake?
Yeye atembeaye gizani,
yeye asiye na nuru,
na alitumainie jina la BWANA,
na amtegemee Mungu wake.
11 [k]Lakini sasa, ninyi nyote mnaowasha
mioto,
na kupeana mienge iwakayo ninyi
kwa ninyi,

[a]**50:1** Kum 24:1; Mk 10:4; Mt 18:25; Amu 3:8; Hos 2:2; Mt 19:7; Neh 5:5; Isa 1:25
[b]**50:2** Mwa 18:14; Kut 14:22; Hes 11:23; 1Sam 8:19; Isa 41:28; Za 68:35; Yer 14:9
[c]**50:3** Isa 5:30; Ufu 6:12; Kut 10:21
[d]**50:4** Kut 4:11-12; Za 88:13; Mt 7:29; Isa 40:29; Mt 11:28
[e]**50:5** Isa 35:5; Eze 2:8; Ebr 10:5; Isa 48:16; Eze 24:3; Mdo 26:19; Mt 26:39
[f]**50:6** Mt 27:30; Isa 53:5; Mao 3:30; Hes 12:14; Mt 26:67; Mk 14:65
[g]**50:7** Isa 41:10; Rum 8:31; Eze 3:8-9; Isa 48:16; 28:16; 29:22
[h]**50:8** Ay 13:19; Rum 8:32-34; 1Kor 4:4; Isa 26:2; 49:4
[i]**50:9** Ay 13:28; Isa 41:10; Ebr 1:11-12; Rum 8:1, 34; Isa 51:8
[j]**50:10** 2Nya 20:20; Isa 49:3; 26:4; 1:19; Hag 1:12; Mdo 26:18; Isa 10:20
[k]**50:11** Mit 26:18; Yak 3:6; Ay 15:20; Isa 65:13-15; Kum 21:22-23

nendeni, tembeeni katika nuru ya moto wenu
na ya mienge mliyoiwasha.
Hili ndilo mtakalolipokea kutoka mkononi mwangu:
Mtalala chini kwa mateso makali.

*Wokovu Wa Milele Kwa Sayuni*

51 [a]"Nisikilizeni, ninyi mnaofuatia haki
na mnaomtafuta Bwana:
Tazameni mwamba ambako mlichongwa,
na mahali pa kuvunjia mawe ambako mlichimbwa;
2 [b]mwangalieni Abrahamu, baba yenu,
na Sara, ambaye aliwazaa.
Wakati nilipomwita alikuwa mmoja tu,
nami nikambariki na kumfanya kuwa wengi.
3 [c]Hakika Bwana ataifariji Sayuni,
naye atayaangalia kwa huruma magofu yake yote;
atayafanya majangwa yake yawe kama Edeni,
nazo sehemu zake zisizolimika ziwe kama bustani ya Bwana.
Shangwe na furaha zitakuwako ndani yake,
shukrani na sauti za kuimba.

4 [d]"Nisikilizeni, watu wangu;
nisikieni, taifa langu:
Sheria itatoka kwangu;
haki yangu itakuwa nuru kwa mataifa.
5 [e]Haki yangu inakaribia mbio,
wokovu wangu unakuja,
nao mkono wangu utaleta hukumu kwa mataifa.
Visiwa vitanitegemea
na kungojea mkono wangu kwa matumaini.
6 [f]Inueni macho yenu mbinguni,
mkaitazame dunia chini;
mbingu zitatoweka kama moshi,
dunia itachakaa kama vazi,
na wakazi wake kufa kama mainzi.
Bali wokovu wangu utadumu milele,
haki yangu haitakoma kamwe.

7 [g]"Nisikieni, ninyi mnaojua lililo sawa,
ninyi watu ambao mna sheria yangu mioyoni mwenu:
Msiogope mashutumu ya wanadamu
wala msitiwe hofu na matukano yao.
8 [h]Kwa maana nondo atawala kama vazi,
nao funza atawatafuna kama sufu.
Lakini haki yangu itadumu milele,
wokovu wangu kwa vizazi vyote."

9 [i]Amka, Amka! Jivike nguvu,
ewe mkono wa Bwana,
Amka, kama siku zilizopita,
kama vile vizazi vya zamani.
Si ni wewe uliyemkata Rahabu vipande vipande,
uliyemchoma yule joka?
10 [j]Si ni wewe uliyekausha bahari,
maji ya kilindi kikuu,
uliyefanya barabara katika vilindi vya bahari
ili waliokombolewa wapate kuvuka?

[a]**51:1** Isa 46:3; Kum 7:13; Mit 26:27; Kum 16:20; Za 94:15; Isa 63:8; Rum 9:30-31; Isa 17:10
[b]**51:2** Mwa 17:6; Ebr 11:11; Mwa 12:2; Isa 29:22; Rum 4:16
[c]**51:3** Isa 40:1; Mwa 13:10; Yer 16:9; Za 102:13; Isa 44:26; Za 51:18; Isa 61:4
[d]**51:4** Kut 6:7; Isa 26:18; 42:4-6; Za 50:7; Isa 3:15; 63:8
[e]**51:5** Isa 35:4; 46:13; Za 98:1; 85:9; Mwa 49:10; Isa 52:10
[f]**51:6** Za 37:20; Lk 21:33; Za 102:25-26; Ebr 1:10-12; Mt 24:35; Isa 54:10
[g]**51:7** Za 37:31; Mt 10:28; Mdo 5:41; Za 119:39; Lk 6:22; Isa 54:4; 50:7
[h]**51:8** Ay 13:28; Yak 5:2; Isa 14:11
[i]**51:9** Kut 32:7; Za 68:30; Ay 26:12; Eze 29:3; Amu 5:12; Mwa 18:14; Za 65:6; 74:13
[j]**51:10** Zek 10:11; Kut 14:21; Ufu 16:12; Kut 15:5, 8, 13; Ay 36:30

11 [a]Wale waliolipiwa fidia na BWANA
watarudi.
Wataingia Sayuni wakiimba;
furaha ya milele itakuwa taji juu
ya vichwa vyao.
Furaha na shangwe zitawapata,
huzuni na kulia kwa uchungu
kutatoweka.

12 [b]"Mimi, naam mimi,
ndimi niwafarijie ninyi.
Ninyi ni nani hata kuwaogopa
wanadamu wanaokufa,
wanadamu ambao ni majani tu,
13 [c]kwamba mnamsahau BWANA
Muumba wenu,
aliyezitanda mbingu
na kuiweka misingi ya dunia,
kwamba mnaishi katika hofu siku
zote
kwa sababu ya ghadhabu ya
mdhalimu,
ambaye nia yake ni kuangamiza?
Iko wapi basi ghadhabu ya
mdhalimu?
14 [d]Wafungwa waliojikunyata kwa
hofu
watawekwa huru karibuni;
hawatafia kwenye gereza lao,
wala hawatakosa chakula.
15 [e]Kwa maana Mimi ndimi BWANA,
Mungu wako,
ambaye huisukasuka bahari ili
mawimbi yake yangurume:
BWANA Mwenye Nguvu Zote ndilo
jina lake.
16 [f]Nimeweka maneno yangu kinywani
mwako
na kukufunika kwa uvuli wa
mkono wangu:
Mimi niliyeweka mbingu mahali
pake,
niliyeweka misingi ya dunia,
niwaambiaye Sayuni,
'Ninyi ni watu wangu.' "

*Kikombe Cha Ghadhabu Ya BWANA*

17 [g]Amka, amka!
Simama, ee Yerusalemu,
wewe uliyekunywa kutoka mkono
wa BWANA
kikombe cha ghadhabu yake,
wewe uliyekunywa mpaka kufikia
machujo yake,
kikombe kile cha kunywea
kiwafanyacho watu
kuyumbayumba.
18 [h]Kati ya wana wote aliowazaa
hakuwepo hata mmoja wa
kumwongoza,
kati ya wana wote aliowalea
hakuwepo hata mmoja wa
kumshika mkono.
19 [i]Majanga haya mawili yamekuja juu
yako:
ni nani awezaye kukufariji?
Maangamizi, uharibifu, njaa na
upanga:
ni nani awezaye kukutuliza?
20 [j]Wana wako wamezimia,
wamelala kwenye mwanzo wa kila
barabara,
kama swala aliyenaswa kwenye
wavu.
Wamejazwa na ghadhabu ya BWANA
na makaripio ya Mungu wako.

21 [k]Kwa hiyo sikiliza hili, wewe
uliyeteswa,
uliyelewa, lakini si kwa mvinyo.

---

[a]**51:11** Isa 35:9; 44:23; 48:20; Ufu 7:17; Yer 31:13; 30:19; Sef 3:17; Isa 30:19
[b]**51:12** Za 118:6; 2Kor 1:3-4; 1Pet 1:24; Isa 15:6; 2Fal 1:15; Isa 2:22; 40:6-7
[c]**51:13** Ay 8:13; 4:17; Isa 17:10; 7:4; Ay 20:7; Isa 45:11; 48:13; 9:4
[d]**51:14** Isa 49:10; Zek 9:11; Isa 42:7
[e]**51:15** Kut 14:21; Isa 43:16; Za 74:13; Yer 31:35; Za 93:3; Isa 13:4
[f]**51:16** Kut 4:12-15; 2Pet 3:13; Kum 18:18; 33:22; Zek 8:8; Eze 14:11; Yer 7:23; 24:7
[g]**51:17** Amu 5:12; Ay 21:20; Ufu 16:19; Za 60:3; 16:5; Mt 20:22; Isa 42:25
[h]**51:18** Ay 31:18; Za 88:18; Isa 49:21; 41:13
[i]**51:19** Isa 40:2; 47:9; 49:13; Yer 14:12; 24:10
[j]**51:20** Yer 14:16; Mao 2:19; Isa 5:25; Ay 18:10; Yer 44:6; Ay 40:11; Kum 28:20
[k]**51:21** Isa 14:32; 29:9; Mao 3:15

22 [a][b]Hili ndilo asemalo BWANA
Mwenyezi wako,
Mungu wako, yeye ambaye
huwatetea watu wake:
“Tazama, nimeondoa mkononi
mwako
kikombe kilichokufanya
uyumbayumbe;
kutoka kikombe hicho,
kikombe cha kunywa cha
ghadhabu yangu,
kamwe hutakunywa tena.
23 [c][d]Nitakiweka mikononi mwa watesi
wako,
wale waliokuambia,
‘Anguka kifudifudi
ili tuweze kutembea juu yako.’
Ukaufanya mgongo wako kama
ardhi,
kama njia yao ya kupita.”

52 [e]Amka, amka, ee Sayuni,
jivike nguvu.
Vaa mavazi yako ya fahari,
ee Yerusalemu, mji mtakatifu.
Asiyetahiriwa na aliye najisi
hataingia kwako tena.
2 [f]Jikung’ute mavumbi yako,
inuka, uketi kwenye kiti cha enzi,
ee Yerusalemu.
Jifungue minyororo iliyo shingoni
mwako,
ee Binti Sayuni uliye mateka.

3 [g]Kwa kuwa hili ndilo asemalo BWANA:

“Mliuzwa pasipo malipo,
nanyi mtakombolewa bila fedha.”

4 [h]Kwa maana hili ndilo asemalo BWANA
Mwenyezi:

“Hapo kwanza watu wangu
walishuka Misri kuishi,
hatimaye, Ashuru wakawaonea.

5 [i]“Basi sasa nina nini hapa?” asema
BWANA.

“Kwa kuwa watu wangu
wamechukuliwa pasipo
malipo,
nao wale wanaowatawala
wanawadhihaki,”
asema BWANA.
“Mchana kutwa
jina langu limetukanwa bila
kikomo.
6 [j]Kwa hiyo watu wangu watalijua
Jina langu;
kwa hiyo katika siku ile watajua
kwamba ndimi niliyetangulia
kulisema.
Naam, ni mimi.”

7 [k]Tazama jinsi miguu ya wale waletao
habari njema
ilivyo mizuri juu ya milima,
wale wanaotangaza amani,
wanaoleta habari njema,
wanaotangaza wokovu,
wauambiao Sayuni,
“Mungu wako anatawala!”
8 [l]Sikiliza! Walinzi wako wanapaza
sauti zao,
pamoja wanapaza sauti zao kwa
furaha.
Wakati BWANA atakaporejea Sayuni,
wataliona kwa macho yao
wenyewe.
9 [m]Pazeni sauti ya nyimbo za furaha
pamoja,
enyi magofu ya Yerusalemu,

[a]**51:22** Yer 50:34; Hab 2:16; Isa 49:25; Yer 25:15; Mt 20:22
[b]**51:22** Yer 50:34; Hab 2:16; Isa 49:25; Yer 25:15; Mt 20:22
[c]**51:23** Yer 49:12; Zek 12:3; Yos 10:24; Isa 14:4; 49:26; Yer 25:15-17, 26; Mik 7:10
[d]**51:23** Yer 49:12; Zek 12:3; Yos 10:24; Isa 14:4; 49:26; Yer 25:15-17, 26; Mik 7:10
[e]**52:1** Isa 51:9; Es 6:8; Ufu 21:2; Yoe 3:17; Zek 3:4; Isa 49:18; Kut 28:2, 40; Neh 1:1
[f]**52:2** Zek 2:7; Isa 29:4; 10:27; Za 81:9; 9:14
[g]**52:3** Za 44:12; Isa 45:13; 1:27; 1Pet 1:18
[h]**52:4** Mwa 46:6; Isa 10:24
[i]**52:5** Eze 36:20; Rum 2:24; Isa 37:23
[j]**52:6** Isa 49:23; Kut 6:3; Isa 41:26; 10:20
[k]**52:7** 2Sam 18:26; Rum 10:15; 1Kor 15:24-25; Lk 2:14; Isa 42:11; 40:9; Efe 6:15
[l]**52:8** Sef 3:9; Eze 3:17; 1Sam 14:16; Isa 56:10; Yer 6:17; Hes 10:36; Zek 8:3
[m]**52:9** Za 98:4; Isa 35:2; Za 74:3; Isa 48:20; Ezr 9:9; Lk 2:25; Isa 51:3

kwa maana BWANA amewafariji
watu wake,
ameikomboa Yerusalemu.
10 [a]Mkono mtakatifu wa BWANA
umefunuliwa
machoni pa mataifa yote,
nayo miisho yote ya dunia itaona
wokovu wa Mungu wetu.

11 [b]Ondokeni, ondokeni, tokeni huko!
Msiguse kitu chochote kilicho
najisi!
Tokeni kati yake mwe safi,
ninyi mchukuao vyombo vya
BWANA.
12 [c]Lakini hamtaondoka kwa haraka,
wala hamtakwenda kwa kukimbia;
kwa maana BWANA atatangulia
mbele yenu,
Mungu wa Israeli atakuwa mlinzi
nyuma yenu.

### *Mateso Na Utukufu Wa Mtumishi*

13 [d]Tazama, mtumishi wangu atatenda
kwa hekima;
atatukuzwa, na kuinuliwa juu, na
kukwezwa sana.
14 [e]Kama walivyokuwa wengi
walioshangazwa naye,
kwani uso wake ulikuwa
umeharibiwa sana
zaidi ya mtu yeyote
na umbo lake kuharibiwa
zaidi ya mfano wa mwanadamu:
15 [f]hivyo atayashangaza mataifa mengi,
nao wafalme watafunga vinywa
vyao kwa sababu yake.
Kwa kuwa yale ambayo
hawakuambiwa, watayaona,
nayo yale wasiyoyasikia,
watayafahamu.

53 [g]Ni nani aliyeamini ujumbe wetu,
na mkono wa BWANA
umefunuliwa kwa nani?
2 [h]Alikua mbele yake kama mche
mwororo
na kama mzizi katika nchi kavu.
Hakuwa na uzuri wala utukufu wa
kutuvutia kwake,
hakuwa na chochote katika
sura yake cha kutufanya
tumtamani.
3 [i]Alidharauliwa na kukataliwa na
wanadamu,
mtu wa huzuni nyingi, ajuaye
mateso.
Kama mtu ambaye watu humficha
nyuso zao,
alidharauliwa, wala
hatukumhesabu kuwa kitu.

4 [j]Hakika alichukua udhaifu wetu
na akajitwika huzuni zetu,
hata hivyo tulidhania kuwa
amepigwa na Mungu,
akapigwa sana naye, na kuteswa.
5 [k]Lakini alitobolewa kwa ajili ya
makosa yetu,
alichubuliwa kwa ajili ya maovu
yetu;
adhabu iliyotuletea sisi amani
ilikuwa juu yake,
na kwa majeraha yake sisi
tumepona.

---

[a]**52:10** Lk 2:30; Za 67:2; Isa 66:18; 2Nya 32:8; Za 44:3; Isa 30:30; Yos 4:24
[b]**52:11** Yer 50:8; 2Kor 6:17; Hes 8:6; 2Tim 2:9; Isa 1:16; 2Nya 36:10; Isa 48:20
[c]**52:12** Kut 14:19; 12:11; Mik 2:13; Yn 10:4
[d]**52:13** Isa 53:3; Mdo 3:13; Yos 1:8; Isa 20:3; 57:15; Flp 2:9
[e]**52:14** Law 26:32; Ay 2:12; 16:16; 18:20; 2Sam 10:4
[f]**52:15** Ebr 9:13; Rum 15:21; Efe 3:4-5; Za 107:42; Amu 18:19; Law 14:7; 16:14-15
[g]**53:1** Isa 28:9; Yn 12:38; Rum 10:16; Za 98:1; Isa 30:30
[h]**53:2** Mk 9:12; Isa 52:14; 2Fal 19:26; Ay 14:7; Isa 4:2; 11:10
[i]**53:3** Ebr 4:15; Mt 16:21; 27:29; 1Sam 2:30; Za 69:29; Kut 1:10; Lk 18:31-33
[j]**53:4** Mt 8:17; Zek 13:7; Yn 19:7; Kum 5:24; Ay 4:5; Yer 23:5-6; Eze 34:23-24; Mik 5:2
[k]**53:5** Kum 32:39; Yn 3:17; 1Pet 2:24-25; 2Nya 7:14; Rum 4:25; 1Kor 15:3; Ebr 9:8; Kut 28:38

6 [a]Sisi sote, kama kondoo, tumepotea,
kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe,
naye Bwana aliweka juu yake
maovu yetu sisi sote.

7 [b]Alionewa na kuteswa,
hata hivyo hakufungua kinywa chake;
aliongozwa kama mwana-kondoo apelekwaye machinjoni,
kama vile kondoo anyamazavyo mbele ya wao wamkataye manyoya,
hivyo hakufungua kinywa chake.
8 [c]Kwa kuonewa na kuhukumiwa aliondolewa.
Nani awezaye kueleza kuhusu kizazi chake?
Kwa maana alikatiliwa mbali na nchi ya walio hai,
alipigwa kwa ajili ya makosa ya watu wangu.
9 [d]Wakamfanyia kaburi pamoja na waovu,
pamoja na matajiri katika kifo chake,
ingawa hakutenda jeuri,
wala hapakuwa na hila kinywani mwake.

10 [e]Lakini yalikuwa ni mapenzi ya Bwana
kumchubua na kumsababisha ateseke.
Ingawa Bwana amefanya maisha yake
kuwa sadaka ya hatia,
ataona uzao wake na kuishi siku nyingi,
nayo mapenzi ya Bwana
yatafanikiwa mkononi mwake.
11 [f]Baada ya maumivu ya nafsi yake,
ataona nuru ya uzima na kuridhika;
kwa maarifa yake, mtumishi wangu mwenye haki
atawafanya wengi kuwa wenye haki,
naye atayachukua maovu yao.
12 [g]Kwa hiyo nitamgawia sehemu miongoni mwa wakuu,
naye atagawana nyara pamoja na wenye nguvu,
kwa sababu aliyamimina maisha yake hadi mauti,
naye alihesabiwa pamoja na wakosaji.
Kwa kuwa alichukua dhambi za wengi,
na kuwaombea wakosaji.

*Utukufu Wa Baadaye Wa Sayuni*

54 [h]"Imba, ewe mwanamke tasa,
wewe ambaye kamwe hukuzaa mtoto;
paza sauti kwa kuimba, piga kelele kwa furaha,
wewe ambaye kamwe hukupata utungu;
kwa sababu watoto wa mwanamke aliyeachwa ukiwa ni wengi
kuliko wa mwanamke mwenye mume,"
asema Bwana.
2 [i]"Panua mahali pa hema lako,
tandaza mapazia ya hema lako uyaeneze mbali,
wala usiyazuie;

---

[a]**53:6** Za 119:176; 1Pet 2:25
[b]**53:7** Mdo 8:32; Mk 14:61; 1Pet 2:23; Isa 49:26; Mt 27:31; Yn 1:29; Za 44:22
[c]**53:8** Za 88:5; Dan 9:26; Mdo 8:32-33; Za 39:8; Mk 14:49
[d]**53:9** Mk 15:43-46; Lk 23:50-53; Isa 42:1-3; Ay 16:17; Ufu 14:5; Yn 19:19, 38-41
[e]**53:10** 2Kor 5:21; Mwa 12:17; Za 22:30; Mdo 2:23; Isa 46:10; Law 5:15; Yn 3:17
[f]**53:11** Yn 10:14-18; Rum 5:18-19; Ay 33:30; Isa 20:3; Mdo 7:52; Yn 1:29; Rum 4:24; Mdo 10:43
[g]**53:12** Flp 2:9; Mt 26:28, 38; 27:38; Lk 23:34; Kut 15:9; Za 119:162; Ebr 9:28; Isa 59:19; Rum 8:34; Mk 15:27; Lk 22:37
[h]**54:1** Isa 49:20; Gal 4:27; Mwa 21:6; Za 98:4; Isa 66:7; 49:20
[i]**54:2** Mwa 26:22; Isa 26:15; Kut 35:18; 39:40; Isa 49:19-20

ongeza urefu wa kamba zako,
imarisha vigingi vyako.
3 [a]Kwa maana utaenea upande wa kuume
na upande wa kushoto;
wazao wako watayamiliki mataifa
na kukaa katika miji yao iliyoachwa ukiwa.

4 [b]"Usiogope, wewe hutaaibika.
Usiogope aibu, wewe hutaaibishwa.
Wewe utasahau aibu ya ujana wako,
wala hutakumbuka tena mashutumu ya ujane wako.
5 [c]Kwa maana Muumba wako ndiye mume wako,
BWANA Mwenye Nguvu Zote ndilo jina lake,
yeye Aliye Mtakatifu wa Israeli ni Mkombozi wako,
yeye anaitwa Mungu wa dunia yote.
6 [d]BWANA atakuita urudi
kana kwamba ulikuwa mke aliyeachwa na kuhuzunishwa rohoni;
kama mke aliyeolewa bado angali kijana
na kukataliwa," asema Mungu wako.
7 [e]"Kwa kitambo kidogo nilikuacha,
lakini kwa huruma nyingi nitakurudisha.
8 [f]Katika ukali wa hasira
nilikuficha uso wangu kwa kitambo,
lakini kwa fadhili za milele
nitakuwa na huruma juu yako,"
asema BWANA Mkombozi wako.

9 [g]"Kwangu mimi jambo hili ni kama siku za Noa,
nilipoapa kuwa maji ya Noa kamwe hayatafunika tena dunia.
Hivyo sasa nimeapa sitawakasirikia ninyi,
kamwe sitawakemea tena.
10 [h]Ijapotikisika milima, na vilima viondolewe,
hata hivyo upendo wangu usiokoma kwenu hautatikisika,
wala agano langu la amani halitaondolewa,"
asema BWANA, mwenye huruma juu yenu.

11 [i]"Ewe mji uliyeteswa, uliyepigwa kwa dhoruba na usiyetulizwa,
nitakujenga kwa almasi, nitaweka misingi yako kwa yakuti samawi.
12 [j]Nitafanya minara yako ya akiki,
malango yako kwa vito ving'aavyo,
nazo kuta zako zote za vito vya thamani.
13 [k]Watoto wako wote watafundishwa na BWANA,
nayo amani ya watoto wako itakuwa kuu.
14 [l]Kwa haki utathibitika:
Kuonewa kutakuwa mbali nawe;
hutaogopa chochote.
Hofu itakuwa mbali nawe;
haitakukaribia wewe.

---

[a]**54:3** Mwa 13:14; Isa 48:19; Ay 12:23; Isa 14:2; 60:4-11; 49:19
[b]**54:4** Isa 30:10; Yoe 2:21; Isa 28:16; Mwa 30:23; Za 25:7; 119:39; Yer 22:21; Isa 47:8
[c]**54:5** Wim 3:3; Isa 41:14; 48:17; Rum 3:29; Hos 2:7-16; Za 149:2; Isa 51:13
[d]**54:6** Isa 49:14-21; 60:15; 62:4; Yer 44:2; Hos 1:10; Kut 20:14; Mal 2:14
[e]**54:7** Ay 14:13; Isa 26:20; 2Kor 4:17; Isa 27:8; Za 71:11; Isa 49:18
[f]**54:8** Isa 9:12; Yer 31:3; Za 92:2; Isa 26:20; Za 25:6; Isa 55:3; 63:7; Hos 2:19
[g]**54:9** Mwa 8:21; Mik 7:18; Eze 39:29; Isa 14:24; Kum 28:20; Isa 49:18
[h]**54:10** Za 46:2; Ebr 12:27; Mwa 9:16; Kut 34:10; Ufu 6:14; Hes 25:12; Isa 55:7
[i]**54:11** Isa 14:32; 29:6; 1Nya 29:2; Ufu 21:18; 21:19-20; Isa 26:18; 28:16; Kut 24:10
[j]**54:12** Ufu 21:21
[k]**54:13** Mik 4:2; Ebr 8:11; Law 26:6; Isa 11:9; 28:9; 48:18; Yn 6:45
[l]**54:14** 2Sam 7:10; Isa 9:4; 17:14; 26:2; Yer 30:20; Sef 3:17; Zek 9:8

15 [a]Kama mtu yeyote akikushambulia,
haitakuwa kwa ruhusa yangu;
yeyote akushambuliaye
atajisalimisha kwako.

16 [b]"Tazama, ni mimi niliyemuumba
mhunzi,
yeye afukutaye makaa kuwa moto,
na kutengeneza silaha inayofaa
kwa kazi yake.
Tena ni mimi niliyemwambia
mharabu
kufanya uharibifu mwingi.
17 [c]Hakuna silaha itakayofanyizwa
dhidi yako
itakayofanikiwa,
nawe utauthibitisha kuwa mwongo
kila ulimi utakaokushtaki.
Huu ndio urithi wa watumishi wa
Bwana
na hii ndiyo haki yao itokayo
kwangu,"
asema Bwana.

*Mwaliko Kwa Wenye Kiu*

55 [d]"Njooni, ninyi nyote wenye kiu,
njooni kwenye maji;
nanyi ambao hamna fedha,
njooni, nunueni na mle!
Njooni, nunueni divai na maziwa
bila fedha na bila gharama.
2 [e]Kwa nini kutumia fedha kwa kitu
ambacho si chakula,
na kutaabikia kitu kisichoshibisha?
Sikilizeni, nisikilizeni mimi na mle
kilicho kizuri,
nazo nafsi zenu zitafurahia utajiri
wa unono.
3 [f]Tegeni sikio mje kwangu,
nisikieni mimi, ili nafsi zenu
zipate kuishi.
Nitafanya agano la milele nanyi,
pendo la uaminifu nililomwahidi
Daudi.
4 [g]Tazama, nimemfanya kuwa shahidi
wa mataifa,
kiongozi na jemadari wa mataifa.
5 Hakika utaita mataifa usiyoyajua,
nayo mataifa yale yasiyokujua
yataharakisha kukujia,
kwa sababu ya Bwana Mungu wako,
yeye Aliye Mtakatifu wa Israeli,
kwa maana amekutukuza."

6 [h]Mtafuteni Bwana maadamu
anapatikana;
mwiteni maadamu yu karibu.
7 [i]Mtu mwovu na aiache njia yake,
na mtu mbaya na ayaache mawazo
yake.
Yeye na amrudie Bwana, naye
atamrehemu,
arudi kwa Mungu wetu, kwa kuwa
atamsamehe bure kabisa.

8 [j]"Kwa kuwa mawazo yangu si
mawazo yenu,
wala njia zenu si njia zangu,"
asema Bwana.
9 [k]"Kama vile mbingu zilivyo juu
kuliko dunia,
ndivyo njia zangu zilivyo juu
kuliko njia zenu
na mawazo yangu kuliko mawazo
yenu.
10 [l]Kama vile mvua na theluji
ishukavyo kutoka mbinguni,

---

[a]**54:15** Isa 41:11-16
[b]**54:16** Isa 44:12; 10:5; 13:5
[c]**54:17** Isa 29:8; Mdo 6:10; Isa 45:24-25; 41:11; 56:6-8; Zek 1:20-21; Isa 65:8-9
[d]**55:1** Mao 5:4; Mit 9:5; Ufu 3:18; Yer 2:31; Isa 35:7; Mt 5:6; Lk 5:21; Yn 4:14; Zek 14:8; Hos 14:4; Eze 47:1, 12
[e]**55:2** Yer 12:13; Hag 1:6; Za 22:26; Mhu 6:2; Isa 49:4; Hos 4:10; 8:7
[f]**55:3** Law 18:5; Yn 6:27; Mwa 9:16; Ebr 13:20; Mdo 13:34; Rum 10:5; Isa 54:10
[g]**55:4** 1Tim 6:13; 1Sam 13:14; Eze 34:23-24; Ebr 2:10; 2Nya 7:18
[h]**55:6** Mdo 17:27; Za 32:6; Amo 5:14; Yer 33:3; Isa 9:13; Kum 4:29; 2Nya 15:2
[i]**55:7** Yer 3:12; 26:3; Isa 32:7; Eze 18:32; 2Nya 6:21; 30:6; Eze 18:27-28
[j]**55:8** Isa 53:6; Mik 4:12; Flp 2:5; 4:8
[k]**55:9** Ay 11:8; Za 103:11; Hes 23:19; Isa 40:13-14
[l]**55:10** 2Kor 9:10; Isa 30:23; Mwa 47:23; Za 67:6; Ay 14:9; Law 25:19

nayo hairudi tena huko
bila kunywesha dunia
na kuichipusha na kuistawisha,
hivyo hutoa mbegu kwa mpanzi
na mkate kwa mlaji,
11 [a]ndivyo lilivyo neno langu lile
litokalo kinywani mwangu:
Halitanirudia tupu,
bali litatimiliza lile nililokusudia
na litafanikiwa katika kusudi lile
nililolituma.
12 Mtatoka nje kwa furaha
na kuongozwa kwa amani;
milima na vilima
vitapaza sauti kwa nyimbo mbele
yenu,
nayo miti yote ya shambani
itapiga makofi.
13 [b]Badala ya kichaka cha miiba
itaota miti ya misunobari,
na badala ya michongoma
utaota mhadasi.[c]
Hili litakuwa jambo la kumpatia
BWANA jina,
kwa ajili ya ishara ya milele,
ambayo haitaharibiwa."

*Wokovu Kwa Ajili Ya Wengine*

56 [d]Hili ndilo asemalo BWANA:

"Dumisheni haki
na mkatende lile lililo sawa,
kwa maana wokovu wangu u karibu
na haki yangu itafunuliwa upesi.
2 [e]Amebarikiwa mtu yule atendaye
hili,
mtu yule alishikaye kwa uthabiti,
yeye ashikaye Sabato bila kuinajisi,
auzuiaye mkono wake usifanye
uovu wowote."

3 [f]Usimwache mgeni aambatanaye na
BWANA aseme,
"Hakika BWANA atanitenga na
watu wake."
Usimwache towashi yeyote
alalamike akisema,
"Mimi ni mti mkavu tu."

4 [g]Kwa kuwa hili ndilo asemalo BWANA:

"Kwa matowashi washikao Sabato
zangu,
ambao huchagua kile
kinachonipendeza
na kulishika sana agano langu:
5 [h]hao nitawapa ndani ya Hekalu
langu na kuta zake
kumbukumbu na jina bora
kuliko kuwa na watoto wa kiume
na wa kike:
nitawapa jina lidumulo milele,
ambalo halitakatiliwa mbali.
6 [i]Wageni wanaoambatana na BWANA
ili kumtumikia,
kulipenda jina la BWANA,
na kumwabudu yeye,
wote washikao Sabato bila kuinajisi
na ambao hushika sana agano
langu:
7 [j]hawa nitawaleta kwenye mlima
wangu mtakatifu
na kuwapa furaha ndani ya
nyumba yangu ya sala.
Sadaka zao za kuteketeza na dhabihu
zao
zitakubalika juu ya madhabahu
yangu;

[a]**55:11** Isa 54:10-13; 1Nya 16:33; Za 98:4; Isa 35:2; Za 65:12-13; 96:12-13; 98:8
[b]**55:13** Hes 33:55; Za 102:12; Yer 32:20; Isa 5:6; 41:19; 63:12; Yer 33:9
[c]13 Mhadasi ni aina ya mti ambao huota milimani karibu na Yerusalemu, hutoa harufu nzuri itumikayo kutengeneza manukato; kwa Kiebrania ni "hadas", na ilikuwa inatumika kujenga vibanda wakati wa Sikukuu ya Vibanda (ona pia Neh 8:15).
[d]**56:1** Yer 22:3; Rum 13:11; Za 85:9; Dan 9:24; Yer 23:6; Isa 26:8
[e]**56:2** Kut 20:8-10; Isa 58:3; Za 119:2
[f]**56:3** Law 21:20; Mdo 8:27; Kut 12:43; 1Fal 8:41; Zek 8:20-23; Yer 38:7; Kum 23:3
[g]**56:4** Yer 38:7; Kut 31:13
[h]**56:5** 1Tim 5:13; Isa 60:18; 48:19; 55:13; Ufu 3:12; Hes 32:42; 1Sam 15:12; Isa 47:3
[i]**56:6** 1Nya 22:2; Isa 61:5; Kut 12:43; 1Fal 8:41; Isa 60:7-10
[j]**56:7** Eze 20:40; Rum 12:1; Isa 19:21; Flp 4:18; Mt 21:13; Mk 11:17; Isa 19:21; Lk 19:46

kwa maana nyumba yangu itaitwa
nyumba ya sala kwa mataifa
yote."
8 [a]BWANA Mwenyezi asema, yeye
awakusanyaye
Waisraeli waliohamishwa:
"Bado nitawakusanya wengine kwao
zaidi ya hao ambao
wamekusanywa tayari."

*Mashtaka Ya Mungu Dhidi Ya Waovu*

9 [b]Njooni, enyi wanyama wote wa
kondeni,
njooni mle, ninyi wanyama wote
wa mwituni!
10 [c]Walinzi wa Israeli ni vipofu,
wote wamepungukiwa na maarifa;
wote ni mbwa walio bubu,
hawawezi kubweka;
hulala na kuota ndoto,
hupenda kulala.
11 [d]Ni mbwa wenye tamaa kubwa,
kamwe hawatosheki.
Wao ni wachungaji waliopungukiwa
na ufahamu;
wote wamegeukia njia yao
wenyewe,
kila mmoja hutafuta faida yake
mwenyewe.
12 [e]Kila mmoja hulia, "Njooni, tupate
mvinyo!
Tunywe kileo sana!
Kesho itakuwa kama leo,
au hata bora zaidi."

*Ibada Ya Sanamu Ya Israeli Iliyo Batili*

57 [f]Mwenye haki hupotea,
wala hakuna hata
mmoja awazaye hilo moyoni
mwake;
watu wanaomcha Mungu
huondolewa,
wala hakuna hata mmoja
anayeelewa
kuwa wenye haki wameondolewa
ili wasipatikane na maovu.
2 [g]Wale waendao kwa unyofu
huwa na amani;
hupata pumziko walalapo mautini.

3 [h]"Lakini ninyi:
Njooni hapa, ninyi wana wa
wachawi,
ninyi wazao wa wazinzi na
makahaba!
4 [i]Mnamdhihaki nani?
Ni nani mnayemcheka kwa
dharau,
na kumtolea ndimi zenu?
Je, ninyi si watoto wa waasi,
uzao wa waongo?
5 [j]Mnawaka tamaa katikati ya mialoni
na chini ya kila mti uliotanda
matawi;
mnawatoa kafara watoto wenu
kwenye mabonde
na chini ya majabali yenye
mianya.

6 [k]"Sanamu zilizo katikati ya mawe
laini ya mabondeni ndizo
fungu lenu;
hizo ndizo sehemu yenu.
Naam, kwa hizo mmemimina sadaka
za vinywaji,
na kutoa sadaka za nafaka.
Katika haya yote,
niendelee kuona huruma?

[a]**56:8** Eze 34:12; Yn 10:16; Efe 1:10; Kum 30:4; Isa 11:12; 60:3-11
[b]**56:9** Yer 12:9; Eze 34:5-8; Isa 18:6; Eze 39:17-20
[c]**56:10** Mt 15:14; Eze 3:17; Nah 3:18; Isa 52:8; 62:6; Yer 6:17; 31:6; 14:13-14
[d]**56:11** Yer 23:1; 8:10; Eze 34:2; Mik 3:11; Isa 53:6; Hos 4:7-8; Isa 57:17
[e]**56:12** Za 10:6; Lk 12:18-19; Law 10:9; Mit 23:20; Isa 42:25
[f]**57:1** Eze 21:3; 2Fal 22:20; Za 12:1; Isa 42:25
[g]**57:2** Isa 26:7; Kum 12:13
[h]**57:3** Mal 3:5; Yak 4:4; Yer 2:20; Kut 22:18; Mt 16:4; Isa 1:20
[i]**57:4** Isa 1:2
[j]**57:5** Kum 12:2; 2Fal 16:4; Eze 16:20; Kum 18:10; Isa 1:29; Law 18:21; 18:2; Za 106:37-38
[k]**57:6** 2Fal 17:10; Hab 2:19; Yer 44:18; 19:13; 7:18; 3:9; 7:18; 5:9-29; 9:9; 2:19

7 [a]Umeweka kitanda chako juu kwenye
kilima kirefu kilichoinuka,
huko ulikwenda kutoa dhabihu
zako.
8 [b]Nyuma ya milango yako na miimo
yako
umeweka alama zako za kipagani.
Kwa kuniacha mimi, ulifunua
kitanda chako,
umepanda juu yake na kukipanua
sana;
ulifanya patano na wale ambao
unapenda vitanda vyao,
nawe uliangalia uchi wao.
9 [c]Ulikwenda kwa Moleki[d] ukiwa na
mafuta ya zeituni,
na ukaongeza manukato yako.
Ukawatuma wajumbe wako mbali
sana,
ukashuka kwenye kaburi[e] lenyewe!
10 [f]Ulikuwa umechoshwa na njia zako
zote,
lakini hukusema, 'Hakuna
tumaini.'
Ulipata uhuisho wa nguvu zako,
kwa sababu hiyo hukuzimia.

11 [g]"Ni nani uliyemhofu hivyo na
kumwogopa
hata ukawa mwongo kwangu,
wala hukunikumbuka
au kutafakari hili moyoni mwako?
Si ni kwa sababu nimekuwa kimya
muda mrefu
hata huniogopi?
12 [h]Nitaifunua haki yako na matendo
yako,
nayo hayatakufaidi.
13 [i]Utakapolia kwa kuhitaji msaada,
sanamu zako ulizojikusanyia na
zikuokoe!
Upepo utazipeperusha zote,
pumzi peke yake itazipeperusha,
Lakini mtu atakayenifanya kimbilio
lake,
atairithi nchi
na kuumiliki mlima wangu
mtakatifu."

*Faraja Kwa Wenye Majuto*

14 [j]Tena itasemwa:

"Jengeni, jengeni, itengenezeni njia!
Ondoeni vikwazo katika njia ya
watu wangu."
15 [k]Kwa maana hili ndilo asemalo Aliye
juu, yeye aliyeinuliwa sana,
yeye aishiye milele, ambaye jina
lake ni Mtakatifu:
"Ninaishi mimi mahali palipoinuka
na patakatifu,
lakini pia pamoja na yeye aliye na
roho iliyotubu
na mwenye roho ya unyenyekevu,
ili kuzihuisha roho za wanyenyekevu
na kuihuisha mioyo yao
waliotubu.
16 [l]Sitaendelea kulaumu milele,
wala sitakasirika siku zote,
kwa kuwa roho ya mwanadamu
ingezimia mbele zangu:
yaani pumzi ya mwanadamu
niliyemuumba.

---

[a]**57:7** Yer 3:6; Eze 6:3; 23:41; 20:29; 20:27-28
[b]**57:8** Eze 16:26; 23:7, 18; 23:18
[c]**57:9** Law 18:21; 1Fal 11:5; Wim 4:10; Eze 23:16, 40
[d]9 Moleki alikuwa mungu aliyekuwa anaabudiwa na Waamoni; pia alijulikana kama Malkomu, Maloki au Kemoshi wa Moabu.
[e]9 Kaburi hapa maana yake ni Kuzimu, kwa Kiebrania ni Sheol.
[f]**57:10** Yer 18:12; Mal 3:14; Isa 47:13; Yer 2:25; 1Sam 2:4
[g]**57:11** Mit 29:25; Eze 22:12; Yer 18:15; Es 4:14; Za 50:21; Yer 3:21; 1Fal 1:15; Isa 17:10
[h]**57:12** Eze 16:2; Mik 2:2-8; Isa 29:15; 66:18
[i]**57:13** Za 37:3-9; Yer 30:15; Isa 2:2-3; Yer 22:20; Amu 10:14; Za 118:8; Isa 65:9-11
[j]**57:14** Isa 62:10; Yer 18:15; Isa 11:16
[k]**57:15** Kum 33:27; Ay 6:10; Mik 6:8; Za 90:2; 2Fal 22:19; Zek 2:13; Isa 52:13; Ay 16:19
[l]**57:16** Za 85:5; Mik 7:18; Ebr 12:9; Isa 3:13-14; 54:9; Zek 12:1

17 [a]Nilighadhibika na tamaa yake ya dhambi;
nilimwadhibu, nikauficha uso wangu kwa hasira,
na bado aliendelea katika njia zake za tamaa.
18 [b]Nimeziona njia zake, lakini nitamponya,
nitamwongoza na kumrudishia upya faraja,
19 [c]nikiumba sifa midomoni ya waombolezaji
katika Israeli.
Amani, amani, kwa wale walio mbali
na kwa wale walio karibu,"
asema BWANA. "Nami nitawaponya."
20 [d]Bali waovu ni kama bahari ichafukayo,
ambayo haiwezi kutulia,
mawimbi yake hutupa takataka na matope.
21 [e]Mungu wangu asema,
"Hakuna amani kwa waovu."

*Mfungo Wa Kweli*

58 [f]"Piga kelele, usizuie.
Paza sauti yako kama tarumbeta.
Watangazieni watu wangu uasi wao,
na kwa nyumba ya Yakobo dhambi zao.
2 [g]Kwa maana kila siku hunitafuta,
wanaonekana kutaka kujua njia zangu,
kana kwamba walikuwa taifa linalotenda lililo sawa,
na ambalo halijaziacha amri za Mungu wake.
Hutaka kwangu maamuzi ya haki,
nao hutamani Mungu awakaribie.
3 [h]Wao husema, 'Mbona tumefunga, nawe hujaona?
Mbona tumejinyenyekeza, nawe huangalii?'

"Lakini katika siku ya kufunga kwenu, mnafanya mnavyotaka
na kuwadhulumu wafanyakazi wenu wote.
4 [i]Kufunga kwenu huishia kwenye magomvi na mapigano,
na kupigana ninyi kwa ninyi kwa ngumi za uovu.
Hamwezi kufunga kama mnavyofanya leo
na kutazamia sauti zenu kusikiwa huko juu.
5 [j]Je, hii ndiyo aina ya mfungo niliouchagua,
siku moja tu ya mtu kujinyenyekeza?
Je, ni kwa kuinamisha kichwa chini kama tete,
na kwa kujilaza juu ya nguo ya gunia na majivu?
Je, huo ndio mnaouita mfungo,
siku iliyokubalika kwa BWANA?

6 [k]"Je, hii si ndiyo aina ya mfungo niliyoichagua:
kufungua minyororo ya udhalimu,
na kufungua kamba za nira,
kuwaweka huru walioonewa,
na kuvunja kila nira?

---

[a]**57:17** Isa 56:11; Yer 8:10; Isa 30:15; 53:6; 66:3
[b]**57:18** Kum 32:39; 2Nya 7:14; Isa 49:13; Za 48:14; Isa 42:16; 48:17
[c]**57:19** Isa 51:16; Ebr 13:15; Efe 2:17; Mdo 2:39; Lk 2:14; Isa 32:17; 26:3
[d]**57:20** Ay 18:5-21; Mwa 49:4; Efe 4:14; Yud 13; Za 69:14
[e]**57:21** Isa 26:3; Eze 13:16; Isa 59:8; 48:22
[f]**58:1** Isa 24:20; 40:6; 48:8; Eze 3:17; Isa 57:12
[g]**58:2** Isa 29:13; Yak 4:8
[h]**58:3** Law 16:29; Mal 3:14; Zek 7:5-6; Kut 10:3; 2Nya 6:37; Yer 44:10; Isa 22:13
[i]**58:4** Mal 2:16; Mao 3:44; Mik 3:4; 1Fal 21:9-13; Isa 59:6; Eze 7:11; 8:18; 1Sam 8:18
[j]**58:5** Zek 7:5; 1Fal 21:27; Mt 6:16; Ay 2:8; Isa 36:6
[k]**58:6** Neh 5:10-11; Kum 14:29; Lk 4:19; Yoe 2:12-13; Yer 34:9; Amo 4:1; Isa 9:4

7 [a]Je, sio kushirikiana chakula chako
na wenye njaa
na kuwapatia maskini wasiokuwa
na makao hifadhi,
unapomwona aliye uchi, umvike,
wala si kumkimbia mtu wa nyama
na damu yako mwenyewe?
8 [b]Ndipo nuru yako itajitokeza kama
mapambazuko
na uponyaji wako utatokea upesi;
ndipo haki yako itakapokutangulia
mbele yako,
na utukufu wa BWANA utakuwa
mlinzi nyuma yako.
9 [c]Ndipo utaita, naye BWANA atajibu,
utalia kuomba msaada,
naye atasema: Mimi hapa.

"Kama ukiiondoa nira ya udhalimu,
na kunyoosha kidole na
kuzungumza maovu,
10 [d]nanyi kama mkimkunjulia mtu
mwenye njaa nafsi zenu
na kutosheleza mahitaji ya
walioonewa,
ndipo nuru yenu itakapong'aa gizani,
nao usiku wenu utakuwa kama
adhuhuri.
11 [e]BWANA atakuongoza siku zote,
atayatosheleza mahitaji yako
katika nchi kame,
naye ataitia nguvu mifupa yako.
Utakuwa kama bustani
iliyonyweshwa vizuri,
kama chemchemi ambayo maji
yake hayakauki kamwe.
12 Watu wako watajenga tena magofu
ya zamani
na kuinua misingi ya kale;
utaitwa Mwenye Kukarabati Kuta
Zilizobomoka,
Mwenye Kurejeza Barabara za
Makao.

13 [f]"Kama ukitunza miguu yako isivunje
Sabato,
na kutokufanya kama vile
upendavyo katika siku yangu
takatifu,
kama ukiita Sabato siku ya furaha
na siku takatifu ya BWANA ya
kuheshimiwa,
kama utaiheshimu kwa kutoenenda
katika njia zako mwenyewe,
na kutokufanya yakupendezayo
au kusema maneno ya upuzi,
14 [g]ndipo utakapojipatia furaha yako
katika BWANA,
nami nitakufanya upande juu ya
miinuko ya nchi
na kusherehekea urithi wa Yakobo
baba yako."
Kinywa cha BWANA kimenena haya.

*Dhambi, Toba Na Ukombozi*

59 [h]Hakika mkono wa BWANA si
mfupi hata usiweze kuokoa,
wala sikio lake si zito hata
lisiweze kusikia.
2 [i]Lakini maovu yenu yamewatenga
ninyi na Mungu wenu,
dhambi zenu zimewaficha ninyi uso
wake,
ili asisikie.
3 [j]Kwa maana mikono yenu imetiwa
mawaa kwa damu
na vidole vyenu kwa hatia.
Midomo yenu imenena uongo,
nazo ndimi zenu zimenong'ona
mambo maovu.

---

[a]**58:7** Ay 22:7; Dan 4:27; Ebr 13:12; Ay 31:19-20; Mwa 29:14; Mt 25:36; Eze 18:16
[b]**58:8** Isa 9:2; 30:26; Kut 14:19; Ay 11:17; Isa 26:2
[c]**58:9** Mit 6:13; Za 50:12; 12:2; Isa 59:13; Ay 8:6; Dan 9:20; Zek 10:6
[d]**58:10** Kum 15:7-8; Ay 11:17; Isa 42:16
[e]**58:11** Za 104:28; Wim 4:15; Yn 4:14; Za 48:14; Isa 42:16; 48:7; Za 68:1; 72:6
[f]**58:13** Law 19:20; Kut 20:8; Za 37:4; Isa 56:2
[g]**58:14** Ay 22:26; Kum 32:13; Isa 1:20; Za 105:10-11
[h]**59:1** Hes 11:23; Isa 50:2; 30:19; 41:20; 58:9; 65:24
[i]**59:2** Za 18:41; Yn 9:31; Yer 11:11; Isa 58:4; Eze 39:23; Yer 5:25
[j]**59:3** 2Fal 21:16; Eze 22:9; Rum 3:15; Isa 1:15; Za 7:3; Isa 3:8

4 [a]Hakuna hata mmoja anayedai kwa haki;
hakuna hata mmoja anayetetea shauri lake kwa haki.
Wanategemea mabishano matupu na kusema uongo,
huchukua mimba ya magomvi na kuzaa uovu.
5 [b]Huangua mayai ya nyoka wenye sumu kali
na kutanda wavu wa buibui.
Yeyote alaye mayai yao atakufa,
na wakati moja lianguliwapo, nyoka hutoka humo.
6 [c]Utando wao wa buibui haufai kwa nguo;
hawawezi kujifunika kwa kile walichokitengeneza.
Matendo yao ni matendo maovu,
vitendo vya jeuri vipo mikononi mwao.
7 [d]Miguu yao hukimbilia kwenye dhambi,
ni myepesi kumwaga damu isiyo na hatia.
Mawazo yao ni mawazo maovu;
uharibifu na maangamizi huonekana katika njia zao.
8 [e]Hawajui njia ya amani,
hakuna haki katika mapito yao.
Wameyageuza kuwa njia za upotovu,
hakuna apitaye njia hizo atakayeifahamu amani.

9 [f]Hivyo uadilifu uko mbali nasi,
nayo haki haitufikii.
Tunatazamia nuru, kumbe! Yote ni giza,
tunatazamia mwanga, lakini tunatembea katika giza kuu.
10 [g]Tunapapasa ukuta kama kipofu,
tunapapasa katika njia zetu kama watu wasio na macho.
Adhuhuri tunajikwaa kama wakati wa gizagiza;
katikati ya wenye nguvu, tuko kama wafu.
11 [h]Wote tunanguruma kama dubu;
tunalia kwa maombolezo kama hua.
Tunatafuta haki, kumbe hakuna kabisa;
tunatafuta wokovu, lakini uko mbali.

12 [i]Kwa sababu makosa yetu ni mengi machoni pako,
na dhambi zetu zinashuhudia dhidi yetu.
Makosa yetu yako pamoja nasi daima,
nasi tunayatambua maovu yetu:
13 [j]Uasi na udanganyifu dhidi ya BWANA,
kumgeuzia Mungu wetu kisogo,
tukichochea udhalimu na maasi,
tukinena uongo ambao mioyo yetu imeuhifadhi.
14 [k]Hivyo uadilifu umerudishwa nyuma,
nayo haki inasimama mbali,
kweli imejikwaa njiani,
uaminifu hauwezi kuingia.
15 [l]Kweli haipatikani popote,
na yeyote aepukaye uovu huwa mawindo.

BWANA alitazama naye akachukizwa
kwamba hapakuwepo haki.

---

[a]**59:4** Za 7:14; Yak 1:15; Isa 5:23; Ay 15:31; Isa 44:20; 29:20; Ay 4:8
[b]**59:5** Ay 8:14; Mt 3:7; Isa 11:8
[c]**59:6** Isa 28:20; Mit 4:17; Za 55:9; Isa 58:4
[d]**59:7** 2Fal 21:16; Mik 3:10; Mit 6:17; Rum 3:15-17; Mk 7:21-22
[e]**59:8** Mit 2:15; Isa 57:21; Lk 1:79; Amu 5:6; Rum 3:15-17
[f]**59:9** Yer 8:15; Ay 19:8; Za 107:14; Isa 5:30; 8:20; Lk 1:79
[g]**59:10** Mao 4:14; Sef 1:17; Ay 3:23; Yn 11:10; Kum 28:29; Isa 6:9-10; Mao 3:6
[h]**59:11** Eze 7:16
[i]**59:12** Ezr 9:6; Yer 2:19; Mwa 4:7; Isa 57; 12; 3:9; Yer 51:3
[j]**59:13** Hes 11:20; Za 12:5; Mt 12:34; Mk 7:21-22; Mit 30; 9; Tit 1:16; Isa 48:8
[k]**59:14** Neh 8:1; Isa 48:1; Yer 33:16; Isa 29:21; 1:21
[l]**59:15** Yer 7:28; Dan 8:12; Isa 5:7

[16] [a]Aliona kuwa hakuwepo hata mtu
mmoja,
akashangaa kwamba hakuwepo
hata mmoja wa kuingilia kati;
hivyo mkono wake mwenyewe
ndio uliomfanyia wokovu,
nayo haki yake mwenyewe
ndiyo iliyomtegemeza.
[17] [b]Alivaa haki kama dirii kifuani
mwake,
na chapeo ya wokovu kichwani
mwake,
alivaa mavazi ya kisasi
naye akajifunga wivu kama joho.
[18] [c]Kulingana na kile walichokuwa
wametenda,
ndivyo atakavyolipa
ghadhabu kwa watesi wake
na kisasi kwa adui zake,
atavilipa visiwa sawa na
wanavyostahili.
[19] [d]Kuanzia magharibi, watu
wataliogopa jina la BWANA
na kuanzia mawio ya jua,
watauheshimu utukufu wake.
Wakati adui atakapokuja kama
mafuriko,
Roho wa BWANA atainua kiwango
dhidi yake na kumshinda.

[20] [e]"Mkombozi atakuja Sayuni,
kwa wale wa Yakobo
wanaozitubu dhambi zao,"
asema BWANA.

[21] [f]"Kwa habari yangu mimi, hili ndilo
agano langu nao," asema BWANA. "Roho
wangu, aliye juu yenu, na maneno yangu
ambayo nimeyaweka katika vinywa vyenu,
havitaondoka vinywani mwenu, wala
kutoka vinywani mwa watoto wenu, wala
kutoka vinywani mwa wazao wao, kuanzia
sasa na hata milele," asema BWANA.

*Utukufu Wa Sayuni*

60 [g]"Ondoka, angaza, kwa kuwa nuru
yako imekuja
na utukufu wa BWANA umezuka
juu yako.
[2] [h]Tazama, giza litaifunika dunia
na giza kuu litayafunika mataifa,
lakini BWANA atazuka juu yako
na utukufu wake utaonekana juu
yako.
[3] [i]Mataifa watakuja kwenye nuru yako
na wafalme kwa mwanga wa
mapambazuko yako.

[4] [j]"Inua macho yako na utazame
pande zote:
Wote wanakusanyika na kukujia,
wana wako wanakuja toka mbali,
nao binti zako wanabebwa
mikononi.
[5] [k]Ndipo utatazama na kutiwa nuru,
moyo wako utasisimka na kujaa
furaha,
mali zilizo baharini zitaletwa kwako,
utajiri wa mataifa utakujilia.
[6] [l]Makundi ya ngamia yatajaa katika
nchi yako,
ngamia vijana wa Midiani na Efa.
Nao wote watokao Sheba watakuja,
wakichukua dhahabu na uvumba
na kutangaza sifa za BWANA.

---

[a]**59:16** Isa 41:28; 65:3; Za 98:1; Isa 53:12; 46:13
[b]**59:17** Efe 6:14; 1The 5:8; Ay 27:6; Eze 5:13; Efe 6:17; Isa 63:3
[c]**59:18** Hes 10:35; Isa 34:8; Mt 16:27
[d]**59:19** Isa 49:12; Za 113:3; Ufu 12:15; Mt 8:11; Za 97:6
[e]**59:20** Yer 35:15; Mdo 2:38-39; Rum 11:26; Ay 19:25; Isa 52:8; Yoe 3:21; Yer 35:15
[f]**59:21** Isa 44:3; Ebr 8:10; Eze 36:37; Mwa 9:16; Kum 29:14; Isa 42:6; Kut 4:15
[g]**60:1** Isa 52:2; Yn 8:12; Mal 4:2; Za 36:9; Efe 5:14; Za 118:27; Ufu 21:11; Kut 16:7
[h]**60:2** Yer 13:16; Kol 1:13; 1Sam 2:9; Za 82:5; Isa 8:20; Za 107:14
[i]**60:3** Mt 2:1-11; Isa 49:23; Ufu 21:24; Isa 44:5; 45:14; 42:6
[j]**60:4** Isa 11:12; 43:6; 49:20-22; Yer 30:10; Isa 43:6
[k]**60:5** Rum 11:25; Kut 34:29; Isa 35:2; 65:13; 66:14; Zek 10:7; Kum 33:19; Amu 3:15; Ufu 21; 6
[l]**60:6** Mwa 25:2-4; Yer 6:20; Za 72:10; Mt 2:11; Amu 6:5; Isa 42:10

7 [a]Makundi yote ya Kedari
yatakusanyika kwako,
kondoo dume wa Nebayothi
watakutumikia,
watakubalika kama sadaka juu ya
madhabahu yangu,
nami nitalipamba Hekalu langu
tukufu.

8 [b]"Ni nani hawa warukao kama
mawingu,
kama hua kuelekea kwenye viota
vyao?
9 [c]Hakika visiwa vinanitazama,
merikebu za Tarshishi[d] ndizo
zinazotangulia,
zikiwaleta wana wenu kutoka mbali,
wakiwa na fedha na dhahabu zao,
kwa heshima ya BWANA, Mungu
wenu,
yeye Aliye Mtakatifu wa Israeli,
kwa maana amekujalia utukufu.

10 [e]"Wageni watazijenga upya kuta
zako,
na wafalme wao watakutumikia.
Ingawa katika hasira nilikupiga,
lakini katika upendeleo wangu
nitakuonyesha huruma.
11 [f]Malango yako yatakuwa wazi siku
zote,
kamwe hayatafungwa, mchana
wala usiku,
ili watu wapate kukuletea utajiri wa
mataifa:
wafalme wao wakiongoza
maandamano ya ushindi.
12 [g]Kwa maana taifa au ufalme ule
ambao hautakutumikia
utaangamia;
utaharibiwa kabisa.

13 [h]"Utukufu wa Lebanoni utakujilia,
msunobari, mvinje pamoja na
mteashuri,
ili kupapamba mahali pangu
patakatifu,
nami nitapatukuza mahali pa
miguu yangu.
14 [i]Wana wa wale waliokuonea
watakuja wakisujudu mbele
yako,
wote wanaokudharau watasujudu
kwenye miguu yako,
nao watakuita Mji wa BWANA,
Sayuni ya Aliye Mtakatifu wa
Israeli.

15 [j]"Ingawa umeachwa na kuchukiwa,
bila yeyote anayesafiri ndani yako,
nitakufanya kuwa fahari ya milele,
na furaha ya vizazi vyote.
16 [k]Utanyonya maziwa ya mataifa,
na kunyonyeshwa matiti ya
wafalme.
Ndipo utakapojua kwamba Mimi,
BWANA, ni Mwokozi wako,
Mkombozi wako, niliye Mwenye
Nguvu wa Yakobo.
17 [l]Badala ya shaba nitakuletea
dhahabu,
na fedha badala ya chuma.
Badala ya mti nitakuletea shaba,
na chuma badala ya mawe.
Nitafanya amani kuwa mtawala
wako,
na haki kuwa mfalme wako.

---

[a]**60:7** Mwa 25:13; Hag 2:3-9; Isa 18:7; Sef 3:10; Eze 20:40; 43:27; Isa 19:21
[b]**60:8** Isa 49:21; 19:1
[c]**60:9** Mwa 10:4; Isa 2:16; 14:2; Yer 30:19; Isa 43:6; Gal 4:26; 1Fal 10:22
[d]9 Au: za biashara (ona pia 1Fal 10:22; 22:48; 2Nya 9:21; 20:36; Isa 2:16).
[e]**60:10** Ezr 1:2; Ufu 21:24; Za 102:13; Isa 54:8; Kut 1:11; Isa 14:1-2; 56:6
[f]**60:11** Mik 2:13; Ufu 21:25-26; Isa 2:12; 61:6; Za 24:7
[g]**60:12** Isa 11:14; Zek 14:17; Za 2:12; Dan 2:34; Mwa 27:29
[h]**60:13** Isa 35:2; Ezr 3:7; 1Nya 28:2; Isa 41:19
[i]**60:14** Mwa 27:29; Ufu 3:9; Ebr 12:22; Isa 14:9; 1:12
[j]**60:15** Isa 6:12; 54:6; Za 126:5; Isa 65:18; 1:7-9; Kut 14:30; Isa 33:8
[k]**60:16** Eze 34:30; Kut 6:2; Isa 66:11-12; Ay 19:25; Isa 59:20; Kut 14:30
[l]**60:17** 1Fal 10:21; Za 85:8; Isa 66:12; 9:7; Hag 2:9

18 [a]Jeuri hazitasikika tena katika nchi yako,
wala maangamizi au uharibifu ndani ya mipaka yako,
lakini utaita kuta zako Wokovu,
na malango yako Sifa.
19 [b]Jua halitakuwa tena nuru yako mchana,
wala mwangaza wa mwezi hautakuangazia,
kwa maana BWANA atakuwa nuru yako ya milele,
naye Mungu wako atakuwa utukufu wako.
20 [c]Jua lako halitazama tena,
nao mwezi wako hautafifia tena;
BWANA atakuwa nuru yako milele,
nazo siku zako za huzuni zitakoma.
21 [d]Ndipo watu wako wote watakuwa waadilifu,
nao wataimiliki nchi milele.
Wao ni chipukizi nililolipanda,
kazi ya mikono yangu,
ili kuonyesha utukufu wangu.
22 [e]Aliye mdogo kwenu atakuwa elfu,
mdogo kuliko wote atakuwa taifa lenye nguvu.
Mimi ndimi BWANA;
katika wakati wake nitayatimiza haya upesi."

*Mwaka Wa Upendeleo Wa BWANA*

61 [f]Roho wa BWANA Mwenyezi yu juu yangu,
kwa sababu BWANA amenitia mafuta
kuwahubiria maskini habari njema.
Amenituma kuwaganga waliovunjika moyo,
kuwatangazia mateka uhuru wao,
na hao waliofungwa
habari za kufunguliwa kwao;
2 [g]kutangaza mwaka wa BWANA uliokubaliwa,
na siku ya kisasi ya Mungu wetu,
kuwafariji wote waombolezao,
3 [h]na kuwapa mahitaji
wale wanaohuzunika katika Sayuni,
ili kuwapa taji ya uzuri badala ya majivu,
mafuta ya furaha badala ya maombolezo,
vazi la sifa badala ya roho ya kukata tamaa.
Nao wataitwa mialoni ya haki,
pando la BWANA,
ili kuonyesha utukufu wake.

4 [i]Watajenga upya magofu ya zamani
na kupatengeneza mahali palipoachwa ukiwa zamani;
watafanya upya miji iliyoharibiwa,
iliyoachwa ukiwa kwa vizazi vingi.
5 [j]Wageni watayachunga makundi yenu,
wageni watafanya kazi katika mashamba yenu,
na kutunza mashamba yenu ya mizabibu.

---

[a]**60:18** Law 26:6; 2Sam 7:10; Yer 33:9; Sef 3:20; Isa 9:4; 49:19; 33:6; 61:11; 62:7
[b]**60:19** Zek 2:5; Za 36:9; Ufu 21:23; 22:5; Za 118:27
[c]**60:20** Amo 8:9; Isa 30:19, 26; Ufu 7:17; Isa 35:10
[d]**60:21** Efe 2:10; Law 10:3; Za 37:11, 22; Zek 8:12; Amo 9:15; Isa 4:3; Yer 32:41; Mt 15:13
[e]**60:22** Mwa 12:2; Kum 1:10; Isa 5:19
[f]**61:1** Isa 11:2; Mdo 4:26; Lk 4:18-19; Zek 9:12; 2Kor 3:17; Isa 50:4; Dan 9:24-26; Ay 5:16
[g]**61:2** Isa 49:8; Mal 4:1-3; Mt 5:4; Isa 1:24; Lk 4:18-19; Ay 5:1; Lk 6:21
[h]**61:3** Isa 60:20-21; 3:23; Ay 2:8; Rut 3:3; Ebr 1:9; Yer 31:13; Za 92:12-13; Mt 15:13
[i]**61:4** Amo 9:14; Yn 15:8; Zek 1:16-17; Isa 44:26; Eze 36:33
[j]**61:5** Isa 14:1-2; Eze 36:33; Isa 56:6

6 [a]Nanyi mtaitwa makuhani wa Bwana,
mtaitwa watumishi wa Mungu wetu.
Mtakula utajiri wa mataifa,
nanyi katika utajiri wao mtajisifu.

7 [b]Badala ya aibu yao
watu wangu watapokea sehemu maradufu,
na badala ya fedheha
watafurahia katika urithi wao;
hivyo watarithi sehemu maradufu katika nchi yao,
nayo furaha ya milele itakuwa yao.

8 [c]"Kwa maana Mimi, Bwana, napenda haki,
na ninachukia unyang'anyi na uovu.
Katika uaminifu wangu nitawapa malipo yao
na kufanya agano la milele nao.
9 [d]Wazao wao watajulikana miongoni mwa mataifa,
na uzao wao miongoni mwa kabila za watu.
Wale wote watakaowaona watatambua
kuwa ni taifa ambalo Bwana amelibariki."

10 [e]Ninafurahia sana katika Bwana,
nafsi yangu inashangilia katika Mungu wangu.
Kwa maana amenivika mavazi ya wokovu,
na kunipamba kwa joho la haki,
kama vile bwana arusi apambavyo kichwa chake kama kuhani,
na kama bibi arusi ajipambavyo kwa vito vyake vya thamani.

11 [f]Kwa maana kama vile ardhi ifanyavyo chipukizi kuota,
na bustani isababishavyo mbegu kuota,
ndivyo Bwana Mwenyezi atafanya haki na sifa
zichipuke mbele ya mataifa yote.

*Jina Jipya La Sayuni*

62 Kwa ajili ya Sayuni sitanyamaza,
kwa ajili ya Yerusalemu sitatulia,
mpaka haki yake itakapoangaza kama mapambazuko,
wokovu wake kama mwanga wa moto.
2 [g]Mataifa wataona haki yako,
nao wafalme wote wataona utukufu wako;
wewe utaitwa kwa jina jipya
lile ambalo kinywa cha Bwana kitatamka.
3 [h]Utakuwa taji ya fahari mkononi mwa Bwana,
taji ya kifalme mkononi mwa Mungu wako.
4 [i]Hawatakuita tena Aliyeachwa,
wala nchi yako kuiita Ukiwa.
Bali utaitwa Hefsiba,[j]
nayo nchi yako itaitwa Beula,[k]
kwa maana Bwana atakufurahia,
nayo nchi yako itaolewa.
5 [l]Kama vile kijana aoavyo mwanamwali,
ndivyo wanao[m] watakavyokuoa wewe;

[a]**61:6** Kut 19:6; Kum 33:19; 1Pet 2:5; Isa 60:1
[b]**61:7** Kum 21:17; Zek 9:12; Isa 29:22; 41:11; 60:21; Za 126:5; Isa 25:9
[c]**61:8** Mwa 9:16; Isa 1:17; 55:3; 5:16; Za 11:7; Ebr 13:20; Isa 42:6
[d]**61:9** Isa 43:5; 48:19; Mwa 12:2; Kum 28:3-12
[e]**61:10** Hab 3:18; Ay 27:6; Isa 49:18; Ufu 21:2; Za 2:11; Isa 7:13; Lk 1:47; Ufu 19:8
[f]**61:11** Za 85:11; Isa 45:8; Mwa 47:23; Isa 58:11
[g]**62:2** Isa 1:26; Za 67:2; Ufu 3:12; Mwa 32:28; Ufu 2:7; Es 4:14; Za 50:12
[h]**62:3** Zek 9:16; 1The 2:19; Isa 28:5
[i]**62:4** Law 26:43; 1Pet 2:10; Hos 2:19; Yer 3:14; Sef 3:17; Mal 3:12; Isa 6:12; 54:6
[j]4 Hefsiba maana yake Yeye ninayemfurahia.
[k]4 Beula maana yake Aliyeolewa.
[l]**62:5** Kum 28:63; Wim 3:11; Isa 65:19; Yer 31:12; Sef 3:17
[m]5 Au: wajenzi wako.

kama bwana arusi amfurahiavyo bibi
arusi wake,
ndivyo Mungu wako
atakavyokufurahia wewe.

6 [a]Nimeweka walinzi juu ya kuta zako,
ee Yerusalemu,
hawatanyamaza mchana wala
usiku.
Ninyi wenye kumwita BWANA,
msitulie,
7 [b]msimwache apumzike hadi
atakapoufanya imara
Yerusalemu
na kuufanya uwe sifa ya dunia.

8 [c]BWANA ameapa kwa mkono wake
wa kuume
na kwa mkono wake wenye
nguvu:
"Kamwe sitawapa tena adui zenu
nafaka zenu kama chakula chao;
kamwe wageni hawatakunywa tena
divai mpya ambayo mmeitaabikia,
9 lakini wale waivunao nafaka wataila
na kumsifu BWANA,
nao wale wakusanyao zabibu
watainywa divai yake
katika nyua za patakatifu pangu."

10 [d]Piteni, piteni katika malango!
Tengenezeni njia kwa ajili ya
watu.
Jengeni, jengeni njia kuu!
Ondoeni mawe.
Inueni bendera kwa ajili ya mataifa.

11 [e]BWANA ametoa tangazo
mpaka miisho ya dunia:
"Mwambie Binti Sayuni,
'Tazama, mwokozi wako anakuja!
Tazama ujira wake uko pamoja naye,
na malipo yake yanafuatana
naye!' "

12 [f]Wataitwa Watu Watakatifu,
Waliokombolewa na BWANA;
nawe utaitwa Aliyetafutwa,
Mji Usioachwa Tena.

*Siku Ya Mungu Ya Kisasi Na Ukombozi*

63 [g]Ni nani huyu anayekuja kutoka
Edomu,
kutoka Bosra, mwenye mavazi
yaliyotiwa madoa mekundu?
Ni nani huyu, aliyevikwa joho la
kifahari,
anayetembea kwa ukuu wa nguvu
zake?

"Mimi ndimi, nisemaye katika haki,
mwenye nguvu wa kuokoa."

2 [h]Kwa nini mavazi yako ni mekundu,
kama ya yule akanyagaye
shinikizo la zabibu?

3 [i]"Nimekanyaga shinikizo la zabibu
peke yangu;
kutoka mataifa hakuna mtu
aliyekuwa pamoja nami.
Nimewaponda kwa miguu katika
hasira yangu
na kuwakanyaga chini katika
ghadhabu yangu;
damu yao ilitia matone kwenye
mavazi yangu,
na kutia madoa nguo zangu zote.
4 [j]Kwa kuwa siku ya kisasi ilikuwa
moyoni mwangu,
mwaka wa ukombozi wangu
umefika.
5 [k]Nilitazama, lakini hakuwepo yeyote
wa kunisaidia,
nilishangaa kwa kuwa hakuwepo
yeyote aliyetoa msaada;

---

[a]**62:6** Eze 3:17; Ebr 13:17; Isa 52:8; Za 132:4
[b]**62:7** Mt 15:21-28; Sef 3:20; Lk 18:1-8; Isa 60:18; Kum 26:19
[c]**62:8** Kum 28:30-33; Yer 5:17; Mwa 22:16; Isa 14:25; 49:18
[d]**62:10** Isa 11:10-16; 57:14; Za 24:7; Isa 60:11
[e]**62:11** Amo 9:14; Kum 12:7; Yoe 2:26; Isa 1:10
[f]**62:12** Za 9:14; Mt 21:5; Isa 35:4; Ufu 22:12; Kum 30:4; Zek 9:9; Isa 40:10
[g]**63:1** Mwa 36:33; Amo 1:12; Yer 42:11; Sef 3:17; 2Nya 28:17; Isa 11:14; Ufu 19:13; Ay 9:4
[h]**63:2** Ufu 19:13; Mwa 49:11
[i]**63:3** Amu 6:11; Ufu 19:15; Mao 1:15; Ufu 19:13; 14:19-20; Za 108:13
[j]**63:4** Isa 1:24; Yer 50:15
[k]**63:5** 2Fal 14:26; Isa 41:28; 59:16; Za 44:3; Yn 16:32; Isa 33:2

hivyo mkono wangu wenyewe ndio
ulionifanyia wokovu,
na ghadhabu yangu mwenyewe
ndiyo iliyonitegemeza.
6 [a]Nilikanyaga mataifa kwa miguu
katika hasira yangu,
katika ghadhabu yangu
niliwalewesha,
na kumwaga damu yao juu ya
ardhi."

*Kusifu Na Kuomba*

7 [b]Nitasimulia juu ya wema wa
Bwana,
kwa matendo ambayo apaswa
kusifiwa,
sawasawa na yote ambayo Bwana
ametenda kwa ajili yetu:
naam, mambo mengi mema
aliyoyatenda
kwa ajili ya nyumba ya Israeli,
sawasawa na huruma zake
na wema wake mwingi.
8 [c]Alisema, "Hakika wao ni watu
wangu,
wana ambao hawatanidanganya";
hivyo akawa Mwokozi wao.
9 [d]Katika taabu zao zote naye
alitaabika,
na malaika wa uso wake
akawaokoa.
Katika upendo wake na rehema zake
aliwakomboa,
akawainua na kuwachukua siku
zote zilizopita.
10 [e]Lakini waliasi,
na kumhuzunisha Roho Mtakatifu
wake.
Hivyo aligeuka na kuwa adui yao,
na yeye mwenyewe akapigana
dhidi yao.
11 [f]Ndipo watu wake wakazikumbuka
siku zilizopita,
siku za Mose na watu wake:
yuko wapi yeye aliyewaleta kupitia
katikati ya bahari,
pamoja na wachungaji wa kundi
lake?
Yuko wapi yule aliyeweka
Roho wake Mtakatifu katikati yao,
12 [g]aliyetuma mkono wake uliotukuka
wenye nguvu
kuwa katika mkono wa kuume wa
Mose,
aliyegawa maji ya bahari mbele yao,
ili kujipatia jina milele,
13 [h]aliyewaongoza kupitia kwenye
vilindi?
Kama farasi katika nchi iliyo wazi,
wao hawakujikwaa,
14 [i]kama ng'ombe washukao bondeni
kwenye malisho,
walipewa pumziko na Roho wa
Bwana.
Hivi ndivyo ulivyowaongoza watu
wako
ili kujipatia mwenyewe jina
tukufu.

15 [j]Tazama chini kutoka mbinguni
ukaone
kutoka kiti chako cha enzi
kilichoinuliwa juu, kitakatifu na
kitukufu.
Uko wapi wivu wako na uweza
wako?
Umetuzuilia wema wako na
huruma zako.
16 [k]Lakini wewe ni Baba yetu,
ingawa Abrahamu hatufahamu sisi
wala Israeli hatutambui;

[a]**63:6** Isa 29:9; Mao 4:21; Isa 34:3; Ay 40:12
[b]**63:7** Isa 54:8; Efe 2:4; Kut 18:9
[c]**63:8** Mdo 9:4; Kut 14:19; 33:14; Kum 7:7-8; Ezr 9:9; Za 28:9; Ay 37:23
[d]**63:9** Kut 14:19; 33:14; Kum 7:7-8; Ezr 9:9; Isa 48:20; Kum 1:31; 32:7; Za 28:9; Ay 37:23
[e]**63:10** Eze 20:8; Mdo 7:39-42; Efe 4:30; Za 106:40; 78:17; Isa 10:4; Yos 10:14
[f]**63:11** Kut 14:22, 30; Hes 11:17; Za 77:20
[g]**63:12** Kut 14:21-22; Isa 11:15; Mwa 49:24
[h]**63:13** Kum 32:12; Yer 31:9; Kut 14:24; Za 119:11
[i]**63:14** Kut 33:14; Kum 12:9
[j]**63:15** Za 80:14; Mao 3:50; 1Fal 22:19; 2:26; Hos 11:8; Kum 26:15; Isa 64:12
[k]**63:16** Ay 14:21; Gal 3:28; Isa 44:6; Kut 4:22; Yer 3:4; Yn 8:41; Isa 59:20

wewe, Ee BWANA, ndiwe Baba yetu,
Mkombozi wetu tangu zamani za kale ndilo jina lako.
17 [a]Ee BWANA, kwa nini unatuacha twende mbali na njia zako,
na kuifanya mioyo yetu migumu hata hatukukuheshimu?
Rudi kwa ajili ya watumishi wako,
yale makabila ambayo ni urithi wako.
18 [b]Kwa maana kwa muda mfupi watu wako walimiliki mahali pako patakatifu,
lakini sasa adui zetu wamepakanyaga mahali patakatifu pako.
19 [c]Sisi tumekuwa kama wale ambao hujawatawala kamwe,
kama wale ambao hawajaitwa kwa jina lako.

64 [d]Laiti ungelipasua mbingu na kushuka chini,
ili milima ingelitetemeka mbele zako!
2 [e]Kama vile moto uteketezavyo vijiti
na kusababisha maji kuchemka,
shuka ukafanye jina lako lijulikane kwa adui zako,
na kusababisha mataifa yatetemeke mbele zako!
3 [f]Kwa maana ulipofanya mambo ya kutisha ambayo hatukuyatazamia,
ulishuka, nayo milima ikatetemeka mbele zako.
4 [g]Tangu nyakati za zamani hakuna yeyote aliyesikia,
hakuna sikio lililotambua,
hakuna jicho lililomwona Mungu mwingine ila wewe,
anayetenda mambo kwa ajili ya wale wamngojeao.
5 [h]Uliwasaidia watu wale watendao yaliyo haki kwa furaha,
wale wazikumbukao njia zako.
Lakini wakati tulipoendelea kutenda dhambi kinyume na njia zako,
ulikasirika.
Tutawezaje basi kuokolewa?
6 [i]Sisi sote tumekuwa kama mtu aliye najisi,
nayo matendo yetu yote ya uadilifu ni kama matambaa machafu;
sisi sote tunasinyaa kama jani,
na kama upepo maovu yetu hutupeperusha.
7 [j]Hakuna yeyote anayeliitia jina lako
wala anayejitahidi kukushika,
kwa kuwa umetuficha uso wako
na kutuacha tudhoofike kwa sababu ya dhambi zetu.

8 [k]Lakini, Ee BWANA, wewe ndiwe Baba yetu.
Sisi ni udongo, wewe ndiye mfinyanzi;
sisi sote tu kazi ya mkono wako.
9 [l]Ee BWANA, usikasirike kupita kiasi,
usizikumbuke dhambi zetu milele.
Ee Bwana, utuangalie, twakuomba,
kwa kuwa sisi sote tu watu wako.
10 [m]Miji yako mitakatifu imekuwa jangwa;
hata Sayuni ni jangwa,
Yerusalemu ni ukiwa.
11 [n]Hekalu letu takatifu na tukufu,

[a]**63:17** Isa 6:10; 29:13; Hes 10:36; Mt 13:15; Mwa 20:13; Mao 3:9; Kut 4:21; 34:9
[b]**63:18** Law 26:31; Dan 8:24; Za 74:3-8; Kum 4:26; Isa 28:18; Lk 21:24; Dan 8:13
[c]**63:19** Isa 43:7; Yer 14:9
[d]**64:1** Kut 19:18; Mik 1:3; Za 18:9
[e]**64:2** Za 119:120; Yer 5:22; Isa 30:27; Yer 33:9
[f]**64:3** Za 65:5; 18:7
[g]**64:4** Za 31:19; Isa 30:18; 1Kor 2:9-10; Kol 1:26-27; Isa 43:10-11; 30:18
[h]**64:5** Isa 26:8; Mdo 10:35; Isa 10:4
[i]**64:6** Isa 46:12; Za 90:5-6; Yer 4:12; Law 12:2
[j]**64:7** Eze 22:30; Yer 8:6; Isa 9:18; Eze 22:18-22; Isa 41:28; Kum 31:18; Za 14:4
[k]**64:8** Yer 18:6; Kut 4:22; Isa 63:16; 29:16; Yer 3:4; Rum 9:20-21; Ay 10:3
[l]**64:9** Isa 54:8; Mao 5:22; Isa 43:25; Za 100:3; Isa 51:4; 57:17
[m]**64:10** Za 78:54; Isa 1:26; Kum 29:23
[n]**64:11** 2Fal 25:9; Eze 24:21; Mao 1:7-10

mahali ambapo baba zetu
walikusifu wewe,
limechomwa kwa moto,
navyo vitu vyote tulivyovithamini
vimeharibika.
12 [a]Ee BWANA, baada ya haya yote,
utajizuia?
Je, utanyamaza kimya na
kutuadhibu kupita kiasi?

*Hukumu Na Wokovu*

65 [b]"Nilijifunua kwa watu wale
ambao hawakuniulizia.
Nimeonekana na watu wale ambao
hawakunitafuta.
Kwa taifa lile ambalo halikuliita Jina
langu,
nilisema, 'Niko hapa, niko hapa.'
2 [c]Mchana kutwa nimeinyoosha
mikono yangu
kwa watu wakaidi,
wanaokwenda katika njia ambazo si
nzuri,
wafuatao mawazo yao wenyewe:
3 [d]taifa ambalo daima hunikasirisha
machoni pangu,
wakitoa dhabihu katika bustani
na kufukiza uvumba juu ya
madhabahu za matofali;
4 [e]watu waketio katikati ya makaburi
na kukesha mahali pa siri,
walao nyama za nguruwe,
nazo sufuria zao zina mchuzi wa
nyama zilizo najisi,
5 [f]wasemao, 'Kaa mbali; usinikaribie,
kwa maana mimi ni mtakatifu
mno kwako!'
Watu wa aina hiyo ni moshi katika
pua zangu,
ni moto uwakao mchana kutwa.

6 [g]"Tazama, jambo hili hubakia
limeandikwa mbele zangu:
sitanyamaza, bali nitalipiza kwa
ukamilifu;
nitalipiza mapajani mwao:
7 [h]dhambi zenu na dhambi za baba
zenu,"
asema BWANA.
"Kwa sababu walitoa dhabihu za
kuteketezwa juu ya milima
na kunichokoza mimi juu ya
vilima,
nitawapimia mapajani mwao
malipo makamilifu kwa matendo
yao ya zamani."

8 [i]Hili ndilo asemalo BWANA:

"Kama vile divai mpya ingali bado
inapatikana
katika kishada cha zabibu,
nao watu husema, 'Usikiharibu,
kwa kuwa bado kuna kitu kizuri
ndani yake,'
hivyo ndivyo nitakavyofanya kwa
ajili ya watumishi wangu;
sitawaangamiza wote.
9 [j]Nitawaleta wazao kutoka kwa
Yakobo,
na kutoka kwa Yuda wale
watakaomiliki milima yangu,
nao watu wangu wateule watairithi,
nako huko wataishi watumishi
wangu.
10 [k]Sharoni itakuwa malisho
kwa ajili ya makundi ya kondoo,

[a]**64:12** Mwa 43:31; Za 74:10-11; Es 4:14; Za 50:21
[b]**65:1** Rum 10:20; Efe 2:12-13; Rum 9:30; Za 22:27; Hos 1:10; Rum 9:24-26; Isa 43:7
[c]**65:2** Za 78:8; Rum 10:21; Za 81:11-12; Mit 24:2; Isa 66:18
[d]**65:3** Isa 1:29; Law 17:5; Ay 1:11; Yer 41:5; Eze 23:41; Yer 44:17
[e]**65:4** Law 11:7; Isa 8:19; Law 19:31; Kum 18:11
[f]**65:5** Za 40:4; Lk 7:39; Yud 19; Mt 9:11; Lk 18:9-12; Mit 10:26
[g]**65:6** 2Nya 6:23; Kum 32:34; Za 50:3; Yer 16:18; Lk 6:38; Isa 59:18; Za 79:12; Eze 9:10
[h]**65:7** Kut 20:5; Yer 32:18; Law 26:39; Isa 22:14; Mit 10:24; Isa 10:12; 57:7
[i]**65:8** Isa 5:2; 54:17; Kut 4:22; Yer 3:4; Isa 29:16; Rum 9:20-21; Ay 10:3
[j]**65:9** Isa 45:19; Hes 34:13; Amo 9:11-15; Isa 32:18; Yer 50:19
[k]**65:10** 1Nya 27:29; Hos 2:15; Mdo 9:35; Yos 7:26; Isa 35:2; Yer 31:12; Eze 34:13-14

na Bonde la Akori mahali pa
kupumzikia
kwa makundi ya ng'ombe,
kwa ajili ya watu wangu
wanaonitafuta.

11 [a]"Bali kwenu ninyi mnaomwacha
BWANA
na kuusahau mlima wangu
mtakatifu,
ninyi mnaoandaa meza kwa ajili ya
Bahati,[b]
na kujaza mabakuli ya mvinyo
uliochanganywa
kwa ajili ya Ajali,[c]
12 [d]nitawaagiza mfe kwa upanga,
nanyi nyote mtainama chini ili
kuchinjwa;
kwa kuwa niliwaita lakini
hamkuitika,
nilisema lakini hamkusikiliza.
Mlitenda maovu machoni pangu,
nanyi mkachagua mambo yale
yanayonichukiza."

13 [e]Kwa hiyo hili ndilo asemalo BWANA Mwenyezi:

"Watumishi wangu watakula,
lakini ninyi mtaona njaa;
watumishi wangu watakunywa
lakini ninyi mtaona kiu;
watumishi wangu watafurahi,
lakini ninyi mtaona haya.
14 [f]Watumishi wangu wataimba
kwa furaha ya mioyo yao,
lakini ninyi mtalia
kutokana na uchungu wa moyoni,
na kupiga yowe kwa sababu
ya uchungu wa roho zenu.
15 [g]Mtaliacha jina lenu
kuwa laana kwa watu wangu
waliochaguliwa;
BWANA Mwenyezi atawaua ninyi,
lakini watumishi wake atawapa
jina jingine.
16 [h]Yeye aombaye baraka katika nchi
atafanya hivyo kwa Mungu wa
kweli;
yeye aapaye katika nchi
ataapa kwa Mungu wa kweli.
Kwa kuwa taabu za zamani
zitasahaulika
na kufichwa kutoka machoni
pangu.

*Mbingu Mpya Na Dunia Mpya*

17 [i]"Tazama, nitaumba
mbingu mpya na dunia mpya.
Mambo ya zamani hayatakumbukwa,
wala hayatakuja akilini.
18 [j]Lakini furahini na kushangilia daima
katika hivi nitakavyoumba,
kwa kuwa nitaumba Yerusalemu
uwe wa kupendeza,
nao watu wake wawe furaha.
19 [k]Nami nitaifurahia Yerusalemu
na kuwafurahia watu wangu;
sauti ya maombolezo na ya kilio
haitasikika humo tena.

20 [l]"Kamwe hatakuwepo tena ndani
yake
mtoto mchanga atakayeishi siku
chache tu,
au mzee ambaye hataishi
akatimiza miaka yake.

---

[a]**65:11** Eze 23:41; Yer 19:4; 1Kor 10:21; Kum 29:24-25; 32:15; Yer 2:13; 19:4
[b]11 Bahati alikuwa mungu wa Wakaldayo ambaye pia alijulikana kama Gadi.
[c]11 Ajali au Meni alikuwa mungu wa majaliwa.
[d]**65:12** Mit 1:24-25; Yer 7:27; 2Nya 36:15-16; Yer 13:11; Isa 1:20; 30:25; Mik 5:15
[e]**65:13** Isa 1:19; Ay 18:12; Lk 6:25; Isa 33:16; 60:5; 44:9
[f]**65:14** Isa 15:2; Lk 13:28; Za 109:28; Sef 3:14-20; Yak 5:13; Mt 8:12
[g]**65:15** Hes 5:27; Mdo 11:26; Zek 8:13; Za 102:8; Mwa 32:28; Ufu 2:17
[h]**65:16** Za 31:5; Ufu 3:14; Isa 19:18; Kum 29:19; Ay 11:16; Za 63:11
[i]**65:17** 2Kor 5:17; 2Pet 3:13; Yer 3:16; Ufu 7:17; Isa 41:22; 43:18
[j]**65:18** Kum 32:43; Za 98:1-9; Isa 25:9; Ufu 21:2
[k]**65:19** Isa 35:10; 62:5; Ufu 7:17; Kum 30:9; Isa 25:8
[l]**65:20** Mwa 15:15; Mhu 8:12; Zek 8:4; Isa 11:8; Mwa 5:1-32

Yeye atakayekufa akiwa na umri wa miaka mia moja
atahesabiwa kwamba ni kijana tu,
yeye ambaye hatafika miaka mia moja,
atahesabiwa kuwa amelaaniwa.
21 [a]Watajenga nyumba na kuishi ndani yake;
watapanda mashamba ya mizabibu na kula matunda yake.
22 [b]Hawatajenga nyumba, nao watu wengine waishi ndani yake,
au kupanda mazao na wengine wale.
Kwa kuwa kama zilivyo siku za mti,
ndivyo zitakavyokuwa siku za watu wangu,
wateule wangu watafurahia kwa siku nyingi
kazi za mikono yao.
23 [c]Hawatajitaabisha kwa kazi bure,
wala hawatazaa watoto ili wapatwe na majanga,
kwa kuwa watakuwa taifa lililobarikiwa na Bwana,
wao na wazao wao pamoja nao.
24 [d]Kabla hawajaita, nitajibu,
nao wakiwa katika kunena, nitasikia.
25 [e]Mbwa mwitu na mwana-kondoo watalisha pamoja,
naye simba atakula nyasi kama maksai,
lakini mavumbi yatakuwa chakula cha nyoka.
Hawatadhuru wala kuharibu
katika mlima wangu mtakatifu wote,"
asema Bwana.

*Hukumu Na Matumaini*

66 [f]Hili ndilo asemalo Bwana,
"Mbingu ni kiti changu cha enzi,
nayo dunia ni mahali pa kuweka miguu yangu.
Iko wapi nyumba mtakayoijenga kwa ajili yangu?
Mahali pangu pa kupumzikia patakuwa wapi?
2 [g]Je, mkono wangu haukufanya vitu hivi vyote,
hivyo vikapata kuwepo?"
asema Bwana.

"Mtu huyu ndiye ninayemthamini:
yeye ambaye ni mnyenyekevu
na mwenye roho yenye toba,
atetemekaye asikiapo neno langu.
3 [h]Lakini yeyote atoaye dhabihu ya fahali
ni kama yeye auaye mtu,
na yeyote atoaye sadaka ya mwana-kondoo,
ni kama yule avunjaye shingo ya mbwa.
Yeyote atoaye sadaka ya nafaka,
ni kama yule aletaye damu ya nguruwe,
na yeyote afukizaye uvumba wa kumbukumbu,
ni kama yule aabuduye sanamu.
Wamejichagulia njia zao wenyewe,
nazo nafsi zao zinafurahia machukizo yao.
4 [i]Hivyo, mimi pia nitawachagulia mapigo makali,
nami nitaleta juu yao kile wanachokiogopa.

---

[a] **65:21** Isa 32:18; 2Fal 19:29; Eze 28:26; Isa 61:4; 37:30; Amo 9:14
[b] **65:22** Za 92:12-14; 21:4; 91:16; Kum 28:30; Isa 14:1
[c] **65:23** Mwa 12:2; Kum 28:3-12; Mdo 2:39; Hos 9:12; Isa 49:4; 1Kor 15:58; Yer 3:4
[d] **65:24** Dan 9:20-23; 10:12; Mt 6:8; Isa 55:6; Ay 8:6; Zek 10:6; Isa 30:19
[e] **65:25** Mwa 3:14; Rum 16:20; Mik 7:17; Isa 11:6; Dan 2:35; Ay 40:15; 5:23; Isa 2:4
[f] **66:1** 2Nya 6:18; Mt 23:22; Mdo 17:24; 1Fal 8:27; Mt 5:34-35; Za 2:4; 2Sam 7:7
[g] **66:2** Isa 40:26; Mdo 17:24; Ezr 9:4; Mit 28:14; Mdo 7:50; Isa 57:15; Mt 5:3-4; Lk 18:13-14
[h] **66:3** Isa 1:11; Law 2:2; Isa 57:17; Kum 27:15; Eze 8:9-13
[i] **66:4** Mit 10:24; 1Sam 8:19; Mit 1:24; 2Fal 21:2-6; Isa 10:12; 41:28; 65:12

Kwa maana nilipoita, hakuna yeyote
aliyejibu,
niliposema, hakuna yeyote
aliyesikiliza.
Walifanya maovu machoni pangu
na kuchagua lile linalonichukiza."

5 [a]Sikieni neno la BWANA,
ninyi mtetemekao kwa neno lake:
"Ndugu zenu wanaowachukia ninyi
na kuwatenga ninyi kwa sababu
ya Jina langu, wamesema,
'BWANA na atukuzwe,
ili tupate kuona furaha yenu!'
Hata sasa wataaibika.
6 [b]Sikieni hizo ghasia kutoka mjini,
sikieni hizo kelele kutoka
hekaluni!
Ni sauti ya BWANA ikiwalipa adui
zake
yote wanayostahili.

7 [c]"Kabla hajasikia utungu, alizaa;
kabla hajapata maumivu,
alizaa mtoto mwanaume.
8 [d]Ni nani amepata kusikia jambo
kama hili?
Ni nani amepata kuona mambo
kama haya?
Je, nchi yaweza kuzaliwa kwa siku
moja,
au taifa laweza kutokea mara?
Mara Sayuni alipoona utungu,
alizaa watoto wake.
9 [e]Je, nilete mwana hadi wakati wa
kuzaliwa
na nisizalishe?" asema BWANA.
"Je, nifunge tumbo la uzazi
wakati mimi ndiye nizalishaye?"
asema Mungu wako.

10 [f]"Shangilieni pamoja na Yerusalemu
na mfurahi kwa ajili yake,
ninyi nyote mnaompenda,
shangilieni kwa nguvu pamoja naye,
ninyi nyote mnaoomboleza juu
yake.
11 [g]Kwa kuwa mtanyonya na kutosheka
katika faraja ya matiti yake;
mtakunywa sana,
na kuufurahia wingi wa mafuriko
ya ustawi wake."

12 [h]Kwa kuwa hili ndilo asemalo BWANA:

"Nitamwongezea amani kama mto,
nao utajiri wa mataifa kama kijito
kifurikacho;
utanyonya na kuchukuliwa mikononi
mwake
na kubembelezwa magotini pake.
13 [i]Kama mama anavyomfariji mtoto
wake,
ndivyo nitakavyokufariji wewe,
nawe utafarijiwa huko
Yerusalemu."

14 [j]Wakati mtakapoona jambo hili,
mioyo yenu itashangilia,
nanyi mtastawi kama majani;
mkono wa BWANA utajulikana kwa
watumishi wake,
bali ghadhabu yake kali
itaonyeshwa kwa adui zake.
15 [k]Tazama, BWANA anakuja na moto,
magari yake ya vita ni kama
upepo wa kisulisuli,
atateremsha hasira yake kwa
ghadhabu kali,
na karipio lake pamoja na miali ya
moto.

---

[a]**66:5** Za 38:20; Yn 15:18-21; Lk 13:17; Tit 2:13; Ezr 9:4; Isa 60:15; 44:9
[b]**66:6** 1Sam 2:10; Za 68:33; Law 26:28; Isa 65:6; Yoe 3:7
[c]**66:7** Isa 54:1; Ufu 12:5
[d]**66:8** Isa 64:4; Yer 18:13; Isa 49:20, 21
[e]**66:9** Isa 37:3
[f]**66:10** Kum 32:43; Rum 15:10; Za 26:8; Isa 25:9; 57:19; 61:2
[g]**66:11** Hes 11:12; Isa 60:16; Mwa 49:25; Isa 25:6; Hes 25:1
[h]**66:12** Isa 33:21; 48:18; Hes 11:12; Isa 60:4-5; Za 72:3; 119:165; Isa 9:6
[i]**66:13** Isa 40:1; 2Kor 1:4; 1The 2:7; Isa 49:15
[j]**66:14** Eze 37:1; Isa 10:5; 30:27; 25:9; Za 72:16; Isa 54:17; 41:20
[k]**66:15** 2Fal 2:11; Za 68:17; Kum 28:20; Za 39:11; Isa 1:31; 42:25

16 [a]Kwa maana kwa moto na kwa
upanga wake
Bwana atatekeleza hukumu juu
ya watu wote,
nao wengi watakuwa ni wale
waliouawa na Bwana.

17 [b]“Watu wote wanaojiweka wakfu na
kujitakasa wenyewe ili kwenda bustanini,
wakimfuata aliye katikati ya wale ambao
hula nyama za nguruwe na panya pamoja na
vitu vingine vilivyo machukizo, watafikia
mwisho wao pamoja,” asema Bwana.
18 [c]“Nami, kwa sababu ya matendo yao na
mawazo yao, niko karibu kuja na kukusanya
mataifa yote na lugha zote, nao watakuja
na kuuona utukufu wangu.
19 [d]“Nitaweka ishara katikati yao, nami
nitapeleka baadhi ya hao walionusurika
kwa mataifa, hadi Tarshishi, kwa Puli[e]
na Waludi (wanaojulikana kama wapiga
upinde), kwa Tubali na Uyunani, hadi
visiwa vya mbali ambavyo havijasikia juu
ya sifa zangu au kuuona utukufu wangu.
Watatangaza utukufu wangu miongoni mwa
mataifa. 20 [f]Nao watawaleta ndugu zenu
wote, kutoka mataifa yote, mpaka kwenye
mlima wangu mtakatifu katika Yerusalemu
kama sadaka kwa Bwana, juu ya farasi,
katika magari ya vita na magari makubwa,
juu ya nyumbu na ngamia,” asema Bwana.
“Watawaleta, kama Waisraeli waletavyo
sadaka zao za nafaka, katika Hekalu la
Bwana, katika vyombo safi kwa kufuata
desturi za ibada. 21 [g]Nami nitachagua baadhi
yao pia wawe makuhani na Walawi,” asema
Bwana.

22 [h]“Kama vile mbingu mpya na nchi
mpya ninazozifanya zitakavyodumu mbele
zangu,” asema Bwana, “ndivyo jina lenu
na wazao wenu watakavyodumu. 23 [i]Kutoka
Mwezi Mpya hata mwingine, na kutoka
Sabato hadi nyingine, wanadamu wote
watakuja na kusujudu mbele zangu,” asema
Bwana. 24 [j]“Nao watatoka nje na kuona
maiti za wale walioniasi mimi. Funza wao
hawatakufa, wala moto wao hautazimika,
nao watakuwa kitu cha kuchukiza sana kwa
wanadamu wote.”

---

[a]**66:16** Amo 7:4; Eze 24:21; Isa 1:20; 30:30; 13:9-11; Yer 2:35; Eze 36:5; Isa 10:4
[b]**66:17** Isa 65:3; Za 37:20; Isa 1:28-29; Law 11:7, 29
[c]**66:18** Mit 24:2; Isa 65:2; 2:3; Zek 12:3; Kut 16:17; Isa 59:19
[d]**66:19** Lk 2:34; Isa 11:10-11; Mt 24:30; Eze 27:10; 1Nya 16:24; Isa 24:15; Yer 46:9
[e]19 Puli hapa inamaanisha Libya.
[f]**66:20** Isa 52:11; Rum 15:16; Yer 31:23; Eze 34:13; Kum 33:19; Yer 25:22
[g]**66:21** Kut 19:6; 1Pet 2:5-9
[h]**66:22** 2Pet 3:13; Isa 65:17; 1Pet 1:4-5; Isa 48:19; Ebr 12:26-27; Yn 10:27-29
[i]**66:23** Eze 46:1-3; Ufu 15:4; Za 22:29; Zek 14:16; Isa 19:21; 44:5
[j]**66:24** Isa 14:11; 1:31; Mt 25:41; Mk 9:48; Za 110:6; Isa 1:2

# YEREMIA

1 [a]Maneno ya Yeremia mwana wa Hilkia,
mmoja wa makuhani katika mji wa
Anathothi, katika nchi ya Benyamini. 2 Neno
la BWANA lilimjia katika mwaka wa kumi
na tatu wa utawala wa Yosia mwana wa
Amoni mfalme wa Yuda, 3 [b]na pia wakati wa
utawala wa Yehoyakimu mwana wa Yosia
mfalme wa Yuda, mpaka mwezi wa tano wa
mwaka wa kumi na moja wa utawala wa
Sedekia mwana wa Yosia mfalme wa Yuda,
wakati watu wa Yerusalemu walipopelekwa
uhamishoni.

*Wito Wa Yeremia*

4 Neno la BWANA lilinijia, kusema,

5 [c]"Kabla sijakuumba ndani ya tumbo
la mama yako, nilikujua;
kabla hujazaliwa nilikutenga kwa
kazi maalum;
nilikuweka uwe nabii kwa
mataifa."

6 [d]Nami nikasema, "Aa, BWANA
Mwenyezi, sijui kusema, kwani mimi ni
mtoto mdogo tu."
7 Lakini BWANA akaniambia, "Usiseme,
'Mimi ni mtoto mdogo tu.' Utaenda
popote nitakapokutuma na kunena lolote
nitakalokuagiza. 8 [e]Usiwaogope, kwa maana
niko pamoja nawe nikuokoe," asema
BWANA.
9 [f]Kisha BWANA akaunyoosha mkono wake
na kugusa kinywa changu, akaniambia,
"Sasa nimeyaweka maneno yangu kinywani
mwako. 10 [g]Tazama, leo nimekuweka juu ya
mataifa na falme ili kung'oa na kubomoa,
kuharibu na kuangamiza, kujenga na
kupanda."
11 [h]Neno la BWANA likanijia kusema, "Je,
Yeremia unaona nini?"
Nami nikajibu, "Naona tawi la mti wa
mlozi."
12 [i]BWANA akaniambia, "Umeona vyema
kwa maana ninaliangalia neno langu ili
kuona kwamba limetimizwa."
13 [j]Neno la BWANA likanijia tena, "Unaona
nini?"
Nikajibu, "Naona chungu kinachochemka,
kikiwa kimeinama kutoka kaskazini."
14 [k]BWANA akaniambia, "Kutoka kaskazini
maafa yatamwagwa kwa wote waishio
katika nchi. 15 [l]Nitawaita watu wote wa
falme za kaskazini," asema BWANA.

"Wafalme wao watakuja na kuweka
viti vyao vya enzi
katika maingilio ya malango ya
Yerusalemu,
watakuja dhidi ya kuta zake zote
zinazouzunguka,
na dhidi ya miji yote ya Yuda.
16 [m]Nitatoa hukumu zangu kwa watu
wangu
kwa sababu ya uovu wao wa
kuniacha mimi,
kwa kufukiza uvumba kwa miungu
mingine
na kuabudu kile ambacho mikono
yao imekitengeneza.

17 [n]"Jiandae! Simama useme chochote
nitakachokuamuru. Usiwaogope, la
sivyo nitakufanya uwaogope wao. 18 [o]Leo
nimekufanya mji wenye ngome, nguzo ya
chuma, na ukuta wa shaba ili kusimama
dhidi ya nchi yote: dhidi ya wafalme wa
Yuda, maafisa wake, makuhani wake na

[a]**1:1** Yos 21:18; Yer 32:7-9
[b]**1:3** 2Fal 24:17; Yer 29:2; 52:15; Ezr 5:12; 2Fal 23:34
[c]**1:5** Yer 25:15-26; Za 139:13-16; Yn 10:36
[d]**1:6** Kut 3:11; 4:10; 6:12; 1Fal 3:7
[e]**1:8** Mwa 8:1; Kut 3:12; Eze 2:6; Yer 15:20; Hes 22:20; Mwa 26:3; Yer 26:24
[f]**1:9** Isa 6:7; Kut 4:12
[g]**1:10** Yer 25:15; 18:7-10; 31:4, 28; 12:17; 24:6
[h]**1:11** Yer 24:3; Amo 7:8-9
[i]**1:12** Ay 29:2; Yer 44:27
[j]**1:13** Zek 4:2; 5:2; Yer 24:3
[k]**1:14** Isa 14:31
[l]**1:15** Yer 9:11; 10:22; 39:3; 4:16
[m]**1:16** Mwa 6:5; Yer 4:12; Kum 28:20; Yer 17:13; Kut 20:3; Yer 44:3-4; 19:4; Hes 25:3
[n]**1:17** Kum 31:6; 1Fal 18:46; Eze 2:6; Yer 7:27; 42:4
[o]**1:18** Isa 50:7

watu wa nchi hiyo. 19 [a]Watapigana nawe lakini hawatakushinda, kwa kuwa niko pamoja nawe, nami nitakuokoa," asema BWANA.

*Israeli Amwacha Mungu*

2 [b]Neno la BWANA lilinijia kusema,
2 [c]"Nenda ukahubiri masikioni mwa watu
wa Yerusalemu:

" 'Nakumbuka moyo wako wa uchaji
katika ujana wako,
jinsi ulivyonipenda kama bibi
arusi
na kunifuata katika jangwa lile lote,
katika nchi isiyopandwa mbegu.
3 [d]Israeli alikuwa mtakatifu kwa
BWANA,
kama malimbuko ya kwanza ya
mavuno yake;
wote waliowaangamiza
walihesabiwa kuwa na hatia,
nayo maafa yaliwakumba,' "
asema BWANA.

4 Sikia neno la BWANA, ee nyumba ya
Yakobo,
nanyi nyote jamaa za nyumba ya
Israeli.

5 [e]Hivi ndivyo asemavyo BWANA:

"Je, baba zenu waliona kosa gani
kwangu,
hata wakatangatanga mbali nami
hivyo?
Walifuata sanamu zisizofaa,
nao wenyewe wakawa hawafai.
6 [f]Hawakuuliza, 'Yuko wapi BWANA,
aliyetupandisha kutoka Misri
na kutuongoza kupitia nyika kame,
kupitia nchi ya majangwa na
mabonde,
nchi ya ukame na giza,
nchi ambayo hakuna mtu asafiriye
ndani yake
wala hakuna mtu aishiye humo?'
7 [g]Niliwaleta katika nchi yenye wingi
wa vitu
ili mpate kula matunda yake
na utajiri wa mazao yake.
Lakini mkaja na kuinajisi nchi
yangu,
na kuufanya urithi wangu chukizo.
8 [h]Makuhani hawakuuliza,
'Yuko wapi BWANA?'
Wale wanaoshughulikia sheria
hawakunijua mimi;
viongozi waliasi dhidi yangu.
Manabii walitabiri kwa jina la Baali,
wakifuata sanamu zisizofaa.

9 [i]"Kwa hiyo naleta tena mashtaka
dhidi yako,"
asema BWANA.
"Nami nitaleta mashtaka dhidi ya
watoto wa watoto wako.
10 [j]Vuka, nenda ng'ambo mpaka pwani
ya Kitimu[k] nawe uangalie,
tuma watu waende Kedari,
wachunguze kwa makini,
uone kama kumekuwepo kitu
kama hiki.
11 [l]Je, taifa limebadili miungu yake
wakati wowote?
(Hata ingawa hao si miungu
kamwe.)
Lakini watu wangu wamebadili
Utukufu wao
kwa sanamu zisizofaa kitu.

---

[a]**1:19** Mwa 26:3; Isa 43:2; Mit 20:22; Hes 14:9; Mdo 26:17; Za 129:2
[b]**2:1** Isa 38:4; Eze 1:3
[c]**2:2** Za 71:17; Eze 16:8; Kut 13:21; Hos 2:15; Ufu 2:4; Isa 54:4; Yer 3:4; Kum 1:29
[d]**2:3** Kut 19:6; Yak 1:18; Kum 7:6; Law 23:9-14; Yer 10:25; Ufu 14:4; Yer 30:16; 50:7
[e]**2:5** 2Fal 17:15; Rum 1:21; Isa 44:9; Kum 32:21; 1Sam 12:21; Za 31:9
[f]**2:6** Hos 13:4; Kum 18:5; 32:10; Kut 6:6; Yer 51:43
[g]**2:7** Hes 13:27; Kum 11:10-12; Za 106:34-39; Kum 8:7-9; Yer 7:30; 16:18; Eze 36:17
[h]**2:8** 2Sam 2:12; Rum 2:20; 1Fal 18:22; Yer 23:13; Isa 40:19; Yer 4:22; 3:15; 9:14
[i]**2:9** Isa 3:13; Mik 6:2; Eze 20:35-36; Yer 25:31
[j]**2:10** Mwa 10:4; 25:13
[k]10 Kitimu hapa ni Kipro, kisiwa katika Bahari ya Mediterania.
[l]**2:11** Gal 4:8; Isa 37:19; Za 106:20; Rum 1:23; Kum 4:5-9; 1Sam 4:21; Yer 16:20

12 Shangaeni katika hili, ee mbingu,
nanyi tetemekeni kwa hofu kuu,”
asema BWANA.
13 [a]“Watu wangu wametenda dhambi mbili:
Wameniacha mimi,
niliye chemchemi ya maji yaliyo hai,
nao wamejichimbia visima vyao wenyewe,
visima vilivyobomoka,
visivyoweza kuhifadhi maji.
14 [b]Je, Israeli ni mtumishi, yaani mtumwa kwa kuzaliwa?
Kwa nini basi amekuwa mateka?
15 [c]Simba wamenguruma;
wamemngurumia.
Wameifanya nchi yake kuwa ukiwa;
miji yake imeteketezwa, nayo imeachwa haina watu.
16 [d]Pia watu wa Memfisi[e] na Tahpanhesi[f]
wamevunja taji ya kichwa chako.
17 [g]Je, hukujiletea hili wewe mwenyewe
kwa kumwacha BWANA, Mungu wako
alipowaongoza njiani?
18 [h]Sasa kwa nini uende Misri
kunywa maji ya Shihori?[i]
Nawe kwa nini kwenda Ashuru
kunywa maji ya Mto Frati?
19 [j]Uovu wako utakuadhibu;
kurudi nyuma kwako kutakukemea.
Basi kumbuka, utambue
jinsi lilivyo ovu na chungu kwako
unapomwacha BWANA Mungu wako
na kutokuwa na hofu yangu,”
asema Bwana, BWANA Mwenye Nguvu Zote.

20 [k]“Zamani nilivunja nira yako
na kukatilia mbali vifungo vyako;
ukasema, ‘Sitakutumikia!’
Naam kweli, kwenye kila kilima kirefu
na chini ya kila mti uliotanda matawi yake
ulijilaza kama kahaba.
21 [l]Nilikupanda ukiwa mzabibu ulio bora sana,
mkamilifu na wa mbegu nzuri.
Ilikuwaje basi ukawa kinyume nami,
ukaharibika na kuwa mzabibu mwitu?
22 [m]Hata ujisafishe kwa magadi
na kutumia sabuni nyingi,
bado doa la hatia yako liko mbele zangu,”
asema BWANA Mwenyezi.
23 [n]“Wawezaje kusema, ‘Mimi si najisi,
sijawafuata Mabaali’?
Kumbuka jinsi ulivyotenda kule bondeni;
fikiri uliyoyafanya.
Wewe ni ngamia jike mwenye mbio
ukikimbia hapa na pale,
24 [o]punda-mwitu aliyezoea jangwa,
anayenusa upepo katika tamaa yake kubwa:
katika wakati wake wa kuhitaji mbegu
ni nani awezaye kumzuia?
Madume yoyote yanayomfuatilia
hayana haja ya kujichosha;
wakati wa kupandwa kwake
watampata tu.

[a]**2:13** Za 36:9; Yn 4:14; Yer 17:13; Kum 31:16; Isa 65:11; 12:3
[b]**2:14** Kut 4:22; Yer 31:9
[c]**2:15** Yer 4:7; 50:17; 2Fal 25:9; Law 26:43
[d]**2:16** Isa 19:13; Yer 43:7-9
[e]16 Memfisi kwa Kiebrania ni Nofu.
[f]16 Tahpanhesi ni mji katika nchi ya Misri.
[g]**2:17** Yer 4:18; Isa 1:28; Yer 17:13; 19:4
[h]**2:18** Isa 30:2; Hos 13:3; Eze 17:15; 2Fal 16:7; Hos 5:13; 7:11; Isa 7:20
[i]18 Kijito kinachoelekeza maji katika Mto Naili.
[j]**2:19** Hos 14:4; Isa 59:12; Yer 14:7; Kut 19:5; Ay 20:14; Amo 8:10; Yer 3:11; 19:4
[k]**2:20** Law 26:13; Yer 3:23; Kum 12:2; Yer 5:5; Ay 21:14; Isa 57:7; Eze 16:15; Isa 1:12
[l]**2:21** Kut 15:17; Za 80:8; Mk 12:1; Isa 5:4
[m]**2:22** Za 51:2; Ay 9:30; Mao 1:8, 17; Yer 17:1
[n]**2:23** Yer 23:27; Mwa 3:12-13; Rum 3:19; 2Fal 23:10; Yer 31:22; Mit 30:12; Yer 9:14
[o]**2:24** Mwa 16:12; Yer 14:6; Ay 39:6

25 [a]Usikimbie hadi miguu yako iwe
haina viatu,
na koo lako liwe limekauka.
Lakini ulisema, 'Haina maana!
Ninaipenda miungu ya kigeni,
nami lazima niifuatie.'

26 "Kama vile mwizi aaibikavyo wakati
amekamatwa,
hivyo ndivyo nyumba ya Israeli
inavyoaibishwa:
wao wenyewe, wafalme wao na
maafisa wao,
makuhani wao na manabii wao.
27 [b]Wanaiambia miti, 'Wewe ndiwe
baba yangu,'
nalo jiwe, 'Wewe ndiwe
uliyenizaa.'
Wamenipa visogo vyao
wala hawakunigeuzia nyuso zao;
lakini wakiwa katika taabu,
wanasema,
'Njoo utuokoe!'
28 [c]Iko wapi basi ile miungu
mliyojitengenezea?
Yenyewe na ije kama inaweza
kuwaokoa
wakati mko katika taabu!
Kwa maana mna miungu mingi
kama mlivyo na miji, ee Yuda.

29 [d]"Kwa nini mnaleta mashtaka dhidi
yangu?
Ninyi nyote mmeniasi,"
asema BWANA.
30 [e]"Nimeadhibu watu wako bure tu,
hawakujirekebisha.
Upanga wako umewala manabii
wako
kama simba mwenye njaa.

31 [f]"Enyi wa kizazi hiki, tafakarini neno
la BWANA:

"Je, nimekuwa jangwa kwa Israeli
au nchi ya giza kuu?
Kwa nini watu wangu wanasema,
'Sisi tuko huru kuzurura,
hatutarudi kwako tena'?
32 Je, mwanamwali husahau vito
vyake,
au bibi arusi mapambo yake ya
arusi?
Lakini watu wangu wamenisahau
mimi,
tena kwa siku zisizo na hesabu.
33 Je, wewe una ustadi kiasi gani katika
kufuatia mapenzi!
Hata wale wanawake wabaya
kuliko wote
wanaweza kujifunza kutokana na
njia zako.
34 [g]Katika nguo zako watu huona
damu ya uhai ya maskini wasio na
hatia,
ingawa hukuwakamata wakivunja
nyumba.
Lakini katika haya yote
35 [h]unasema, 'Sina hatia;
Mungu hajanikasirikia.'
Lakini nitakuhukumu kwa sababu
unasema,
'Mimi sijatenda dhambi.'
36 [i]Kwa nini unatangatanga sana,
kubadili njia zako?
Utakatishwa tamaa na Misri
kama ulivyokatishwa na Ashuru.
37 [j]Pia utaondoka mahali hapo
ukiwa umeweka mikono kichwani,
kwa kuwa BWANA amewakataa wale
unaowatumainia;
hutasaidiwa nao.

---

[a]**2:25** Isa 57:10; Kum 32:16; Yer 3:13; 14:10
[b]**2:27** Yer 32:33; Eze 7:22; Isa 26:16; Yer 10:8; 9:3; 1Fal 14:9; 2Nya 29:9
[c]**2:28** Isa 45:20; Kum 32:37; 2Fal 17:29; Isa 40:19
[d]**2:29** Dan 9:11; Mik 3:11; Yer 6:13; Mik 7:2
[e]**2:30** Neh 9:26; 2Nya 36:16; Mdo 7:52; 1The 2:15; Yer 11:21; Law 26:23
[f]**2:31** Isa 45:19; Ay 21:14
[g]**2:34** Yer 19:4; Mit 6:17; Kut 22:2; 2Fal 21:16
[h]**2:35** Mit 28:13; Eze 17:20; 2Sam 12:13; 1Yn 1:8-10; Mit 30:12; Isa 66:16; Yer 25:31
[i]**2:36** Yer 31:22; Hos 5:13; Za 108:12; Isa 30:2-7; Yer 37:7
[j]**2:37** 2Sam 13:19; Yer 37:7

*Israeli Asiye Mwaminifu*

3 [a]“Kama mtu akimpa talaka mkewe,
naye akamwacha na akaolewa
na mtu mwingine,
je, huyo mume aweza kumrudia
tena?
Je, hiyo nchi haitanajisika kabisa?
Lakini umeishi kama kahaba na
wapenzi wengi:
je, sasa utanirudia tena?”
asema Bwana.
2 [b]“Inua macho utazame miinuko iliyo
kame na uone.
Je, pana mahali ambapo
hawajalala nawe?
Uliketi kando ya barabara
ukiwasubiri wapenzi,
ukakaa kama yeye ahamahamaye
jangwani.
Umeinajisi nchi
kwa ukahaba wako na uovu wako.
3 [c]Kwa hiyo mvua imezuiliwa,
nazo mvua za vuli hazikunyesha.
Hata hivyo, una uso usio na haya
kama wa kahaba;
unakataa kutahayari kwa aibu.
4 [d]Je, wewe hujaniita hivi punde tu:
‘Baba yangu, rafiki yangu tangu
ujana wangu,
5 [e]je, utakasirika siku zote?
Je, ghadhabu yako itaendelea
milele?’
Hivi ndivyo unavyozungumza,
lakini unafanya maovu yote
uwezayo.”

*Wito Kwa Ajili Ya Toba*

6 [f]Wakati wa utawala wa Mfalme Yosia,
Bwana aliniambia, “Umeona kile Israeli
asiye mwaminifu amekifanya? Amepanda
juu ya kila kilima kirefu, na chini ya kila
mti uliotanda na amefanya uzinzi huko.
7 [g]Mimi nilifikiri kuwa baada ya kuyafanya
yote haya angelinirudia, lakini hakurudi,
naye dada yake Yuda mdanganyifu aliona
hili. 8 [h]Nilimpa Israeli asiye mwaminifu hati
yake ya talaka, na kumfukuza kwa ajili ya
uzinzi wake wote. Hata hivyo nikaona kuwa
Yuda dada yake mdanganyifu hakuogopa.
Yeye pia alitoka na kufanya uzinzi. 9 [i]Kwa
sababu uasherati wa Israeli haukuwa kitu
kwake, Yuda aliinajisi nchi kwa kuzini na
mawe na miti. 10 [j]Pamoja na hayo yote,
Yuda dada yake mdanganyifu hakunirudia
kwa moyo wake wote, bali kwa kujifanya
tu,” asema Bwana.
11 [k]Bwana akaniambia, “Israeli asiye
mwaminifu ana haki kuliko Yuda
mdanganyifu. 12 [l]Nenda, ukatangaze
ujumbe huu kuelekea kaskazini:

“ ‘Rudi, Israeli usiye mwaminifu,’
asema Bwana,
‘sitakutazama tena kwa uso
uliokunjamana,
kwa kuwa mimi ni mwenye huruma,’
asema Bwana,
‘Sitashika hasira yangu milele.
13 [m]Ungama dhambi zako tu:
kwamba umemwasi Bwana
Mungu wako,
umetapanya wema wako kwa
miungu ya kigeni
chini ya kila mti unaotanda,
nawe hukunitii mimi,’ ”
asema Bwana.

14 [n]“Rudini, enyi watu msio waaminifu,
kwa kuwa mimi ni mume wenu,” asema
Bwana. “Nitawachagua ninyi, mmoja
kutoka kwenye mji, na wawili kutoka kwenye

[a]**3:1** Kum 24:1-4; Lk 15:16, 24; Mwa 3; 17; 2Fal 16; 7; Yer 2:25; Eze 16:26; Hos 2:5, 12
[b]**3:2** Mwa 38:14; Eze 16:25; Kum 12:2; Hes 15:39; Isa 1:21
[c]**3:3** Law 26:19; Kum 11:14; Amo 4; 7; Sef 3:5; Yer 5:25; 14:4; Yoe 1:10; Eze 16:30
[d]**3:4** Kum 32:6; Hos 2:15; Za 89:26; Isa 63:16; Yer 31:9
[e]**3:5** Isa 57:19; Za 103:9
[f]**3:6** Kum 12:2; Hos 4:13; Yer 2:20; 1Nya 3:14; Isa 24:16; Yer 31:22; Eze 20:28
[g]**3:7** Eze 16:46; 2Fal 17:13; Amo 4:8
[h]**3:8** Eze 16:47; 23:11; Yer 11:10; Kum 4:27
[i]**3:9** Law 17:7; Isa 1:21; 57:6; Yer 7:22
[j]**3:10** Yer 12:2; Eze 33:31; Hos 7:14; Isa 31:6; Amo 4:9; Hag 2:17; 2Fal 17:19
[k]**3:11** Eze 16:52; 23:11; Yer 2:19
[l]**3:12** Isa 44:22; 2Fal 17:3-6; Kum 4:30; Za 86:15; Yer 31:21; Eze 14:6; 1Fal 3:26
[m]**3:13** Law 26:40-44; Yer 31:18-20; Lk 15:18-21; 1Yn 1:9; Yer 2:2, 5; Kum 12:2; Yer 14; 20
[n]**3:14** Rum 11:5; Ay 22:23; Hos 2:19; Isa 54:5

ukoo, nami nitawaleta Sayuni. 15 [a]Kisha
nitawapeni wachungaji wanipendezao
moyo wangu, ambao watawaongoza kwa
maarifa na ufahamu. 16 [b]Katika siku hizo,
idadi yenu itakapokuwa imeongezeka
sana katika nchi, watu hawatasema tena,
'Sanduku la Agano la BWANA,'" asema
BWANA. "Halitaingia tena kwenye mawazo
yao wala kukumbukwa, hawatalihitaji wala
halitatengenezwa jingine. 17 [c]Wakati huo,
wataita Yerusalemu kuwa Kiti cha Enzi cha
BWANA, nayo mataifa yote watakusanyika
Yerusalemu kuliheshimu jina la BWANA.
Hawatafuata tena ukaidi wa mioyo yao
miovu. 18 [d]Katika siku hizo, nyumba ya
Yuda itaungana na nyumba ya Israeli,
wao kwa pamoja watakuja kutoka nchi ya
kaskazini hadi nchi niliyowapa baba zenu
kama urithi.

19 [e]"Mimi mwenyewe nilisema,

"'Tazama jinsi nitakavyowatunza
kwa furaha kama wana
na kuwapa nchi nzuri,
urithi ulio mzuri kuliko wa taifa
jingine lolote.'
Nilidhani mngeniita 'Baba,'
na msingegeuka, mkaacha
kunifuata.
20 Lakini kama mwanamke asiye
mwaminifu kwa mumewe,
vivyo hivyo mmekosa uaminifu
kwangu pia, ee nyumba ya
Israeli,"
asema BWANA.

21 [f]Kilio kinasikika juu ya miinuko iliyo
kame,
kulia na kuomboleza kwa watu wa
Israeli,
kwa sababu wamepotoka katika njia
zao
na wamemsahau BWANA Mungu
wao.

22 [g]"Rudini, enyi watu msio waaminifu,
nami nitawaponya ukengeufu
wenu."

"Naam, tutakuja kwako,
kwa maana wewe ni BWANA
Mungu wetu.
23 [h]Hakika zile ghasia za kuabudu
sanamu kwenye vilima
na milimani ni udanganyifu;
hakika katika BWANA, Mungu wetu,
uko wokovu wa Israeli.
24 [i]Tangu ujana wetu miungu ya aibu
imeyala
matunda ya kazi za baba zetu:
makundi yao ya kondoo na ng'ombe,
wana wao na binti zao.
25 [j]Sisi na tulale chini katika aibu yetu,
na fedheha yetu itufunike.
Tumetenda dhambi dhidi ya BWANA
Mungu wetu,
sisi na mababa zetu;
tangu ujana wetu hadi leo
hatukumtii BWANA Mungu wetu."

4 1 [k]"Ikiwa utataka kurudi, ee Israeli,
nirudie mimi,"
asema BWANA.
"Ikiwa utaondoa sanamu zako za
kuchukiza mbele ya macho
yangu
na usiendelee kutangatanga,
2 [l]ikiwa kwa kweli, kwa haki na kwa
unyofu utaapa,
'Kwa hakika kama vile BWANA
aishivyo,'

---

[a]**3:15** Isa 31:4; Mdo 20:28; Efe 4:10; Mdo 13:22
[b]**3:16** Isa 65:17; Yn 4:21-24; Hes 3:31; 1Nya 15:25
[c]**3:17** Za 47:8; Eze 43:7; Za 22:23; 81:12; Yer 18:12; 17:12; 33:16
[d]**3:18** Amo 9:15; Eze 37:19; Yer 16:15; Isa 11:13; Hos 1:11; Yer 30:3; 50:4; Kum 31:7; Kut 4:22
[e]**3:19** Kut 4:22; Isa 63:16; 2Sam 7:14; Za 106:24; Eze 20:6
[f]**3:21** Yer 31:18; Isa 57:11
[g]**3:22** Hos 14:4; Ay 22:23; Isa 30:26; Hos 6:1; Yer 33:6; 2:19
[h]**3:23** Yer 17:14; Za 3:8; Yer 2:20
[i]**3:24** Yer 11:13; Hos 9:10
[j]**3:25** Eze 6:9; Dan 9:7; Za 25:7; Yer 22:21; 31:19; Amu 10:10; 1Fal 8:47; Yer 14:20
[k]**4:1** Yoe 2:12; Ezr 8:5; 2Fal 7:13; 21:4; Kum 4:30; Hos 12:6; Yer 16:18; 35:15
[l]**4:2** Kum 10:20; Hes 14:21; Gal 3:8; Hos 4:15; Mwa 12:2; Isa 19:18; 65:16; Yer 12:16

ndipo mataifa yatakapobarikiwa
naye
na katika yeye watajitukuza."

3 [a]Hili ndilo asemalo BWANA kwa watu
wa Yuda na kwa Yerusalemu:

"Vunjeni mabonge kwenye
mashamba yenu,
wala msipande katikati ya miiba.
4 [b]Jitahirini katika BWANA,
tahirini mioyo yenu,
enyi wanaume wa Yuda
na watu wa Yerusalemu,
la sivyo ghadhabu yangu itatoka kwa
nguvu
na kuwaka kama moto
kwa sababu ya uovu mliotenda,
ikiwaka pasipo wa kuizima.

*Maafa Kutoka Kaskazini*

5 "Tangaza katika Yuda na upige mbiu
katika Yerusalemu na kusema:
'Piga tarumbeta katika nchi yote!'
Piga kelele na kusema:
'Kusanyikeni pamoja!
Tukimbilie katika miji yenye
maboma!'
6 [c]Onyesheni ishara ili kwenda Sayuni!
Kimbilieni usalama pasipo
kuchelewa!
Kwa kuwa ninaleta maafa kutoka
kaskazini,
maangamizi ya kutisha."

7 [d]Simba ametoka nje ya pango lake,
mharabu wa mataifa amejipanga.
Ametoka mahali pake
ili aangamize nchi yenu.
Miji yenu itakuwa magofu
pasipo mtu wa kuishi humo.

8 [e]Hivyo vaeni nguo za magunia,
ombolezeni na kulia kwa huzuni,
kwa kuwa hasira kali ya BWANA
haijaondolewa kwetu.

9 "Katika siku ile," asema BWANA
"mfalme na maafisa watakata
tamaa,
makuhani watafadhaika,
na manabii watashangazwa mno."

10 [f]Ndipo niliposema, "Aa, BWANA
Mwenyezi, umewadanganyaje kabisa
watu hawa na Yerusalemu kwa kusema,
'Mtakuwa na amani,' wakati upanga uko
kwenye koo zetu!"
11 [g]Wakati huo watu hawa na Yerusalemu
wataambiwa, "Upepo wa moto kutoka
miinuko iliyo kame katika jangwa unavuma
kuelekea watu wangu, lakini sio kupepeta
au kutakasa, 12 [h]upepo wenye nguvu sana
kuliko wa kupepeta na kutakasa utakuja
kwa amri yangu. Sasa natangaza hukumu
zangu dhidi yao."

13 [i]Tazama! Anakuja kama mawingu,
magari yake yanakuja kama upepo
wa kisulisuli,
farasi wake wana mbio kuliko tai.
Ole wetu! Tunaangamia!
14 [j]Ee Yerusalemu, usafishe uovu
kutoka moyoni mwako na
uokolewe.
Utaendelea kuficha mawazo
mapotovu mpaka lini?
15 [k]Sauti inatangaza kutoka Dani,
ikipiga mbiu ya maafa kutoka
vilima vya Efraimu.

---

[a]**4:3** Hos 10:12; Mk 4:18
[b]**4:4** Law 26:41; Rum 2:28-29; Sef 2:2; Amo 5:6; Ay 41:21; Kut 32:22; Yer 8:14; Yos 10:20; Yer 5:20; Hes 10:2-7; Ay 39:24
[c]**4:6** Yer 1:13-15; Isa 14:31; Za 74:4; Isa 31:9; Yer 50:2; 11:11; 18:11
[d]**4:7** Dan 7:4; Eze 12:20; Yer 2:15; Isa 6:11; Yer 25:38; Hos 5:14; Nah 2:12; Yer 6:26
[e]**4:8** 1Fal 21:27; Yer 30:24; Isa 22:12; 3:24; Yer 6:26; Eze 7:18; Yer 7:29; 9:20
[f]**4:10** Eze 14:9; Kut 5:23; 2The 2:11; Isa 63:17; Yer 6:14; 8:11; Eze 13:10; Mik 3:5
[g]**4:11** Mwa 41:6; Hos 13:15; Eze 17:10; Law 26:33; Ay 1:19
[h]**4:12** Isa 64:6; Yer 1:16
[i]**4:13** Isa 5:28; 2Sam 22:10; Eze 26:10; Kum 28:49; Mao 4:19; Isa 66:15
[j]**4:14** Rut 3; 3; Yak 4:8; Za 51:2; Isa 45:22; Za 6:3
[k]**4:15** Yer 8:16; Mwa 30:6; Yer 31:6

16 “Waambie mataifa jambo hili,
piga mbiu hii dhidi ya Yerusalemu:
‘Jeshi la kuzingira linakuja kutoka nchi ya mbali,
likipiga kelele ya vita dhidi ya miji ya Yuda.
17 [a]Wamemzunguka kama watu walindao shamba,
kwa sababu amefanya uasi dhidi yangu,’ ”
asema BWANA.
18 [b]“Mwenendo wako na matendo yako mwenyewe
yameleta haya juu yako.
Hii ndiyo adhabu yako.
Tazama jinsi ilivyo chungu!
Tazama jinsi inavyochoma moyo!”

19 [c]Ee mtima wangu, mtima wangu!
Ninagaagaa kwa maumivu.
Ee maumivu makuu ya moyo wangu!
Moyo wangu umefadhaika ndani yangu,
siwezi kunyamaza.
Kwa sababu nimesikia sauti ya tarumbeta,
nimesikia kelele ya vita.
20 [d]Maafa baada ya maafa,
nchi yote imekuwa magofu.
Kwa ghafula mahema yangu yameangamizwa,
makazi yangu kwa muda mfupi.
21 [e]Hata lini nitaendelea kuona bendera ya vita
na kusikia sauti za tarumbeta?

22 [f]“Watu wangu ni wapumbavu,
hawanijui mimi.
Ni watoto wasio na akili,
hawana ufahamu.
Ni hodari kutenda mabaya,
hawajui kutenda yaliyo mema.”

23 [g]Niliitazama dunia,
nayo haikuwa na umbo tena ni tupu;
niliziangalia mbingu,
mianga ilikuwa imetoweka.
24 [h]Niliitazama milima, nayo ilikuwa ikitetemeka,
vilima vyote vilikuwa vikiyumbayumba.
25 [i]Nilitazama, wala watu hawakuwepo;
kila ndege wa angani alikuwa ameruka zake.
26 Nilitazama, hata nchi iliyokuwa imestawi vizuri imekuwa jangwa,
miji yake yote ilikuwa magofu
mbele za BWANA,
mbele ya hasira yake kali.
27 [j]Hivi ndivyo BWANA asemavyo:
“Nchi yote itaharibiwa,
ingawa sitaiangamiza kabisa.
28 [k]Kwa hiyo dunia itaomboleza
na mbingu zilizo juu zitakuwa giza,
kwa sababu nimesema nami sitarudi nyuma,
nimeamua na wala sitageuka.”

29 [l]Kwa sauti ya wapanda farasi na wapiga upinde
kila mji unakimbia.
Baadhi wanakimbilia vichakani,
baadhi wanapanda juu ya miamba.
Miji yote imeachwa,
hakuna aishiye ndani yake.

[a]**4:17** 2Fal 25:1-4; 1Sam 12:15; Yer 5:23
[b]**4:18** Za 107:17; Ay 20:6-11; Yer 2:17-19; Isa 1:28; Yer 5:25
[c]**4:19** Isa 16:11; Mao 1:20; Hes 10:9; Yer 20:9; Sef 1:16; Isa 22:4; Yer 6:24
[d]**4:20** Kum 31:17; Za 42:7; Hes 24:5; Mao 2:4; Yer 10:20
[e]**4:21** Hes 2:2; Isa 18:3; Yos 6:20; Hos 5:8
[f]**4:22** 1Kor 14:20; Yer 5:21; 13:23; Za 36:3; Rum 16:19; Yer 5:21; 10:8; Za 14:4
[g]**4:23** Ay 9:7; 30:26; Isa 5:30; 59:9; Mao 3:2
[h]**4:24** Eze 38:20; Ay 9:6; Isa 5:25; Kut 19:18
[i]**4:25** Hos 4:3; Sef 1:3; Yer 7:20
[j]**4:27** Amo 9:8; Yer 5:10; 12:12; Eze 20:17; Yer 46:28
[k]**4:28** Yer 14:2; Hos 4:3; Hes 23:19; Isa 5:30; Yer 30:24; 23:20; 12:4-11
[l]**4:29** Yer 8:16; Isa 6:12; 2Fal 25:4; Yer 6:23; 1Sam 26:20; Kut 33:22

30 [a]Unafanya nini, ewe uliyeharibiwa?
Kwa nini unajivika vazi jekundu
na kuvaa vito vya dhahabu?
Kwa nini unapaka macho yako
rangi?
Unajipamba bure.
Wapenzi wako wanakudharau,
wanautafuta uhai wako.

31 [b]Nasikia kilio kama cha mwanamke
katika utungu wa kuzaa,
kilio cha uchungu kama cha
anayemzaa
mtoto wake wa kwanza:
kilio cha Binti Sayuni akitweta ili
aweze kupumua,
akiinua mikono yake, akisema,
"Ole wangu! Ninazimia;
maisha yangu yamekabidhiwa kwa
wauaji."

*Hakuna Hata Mmoja Aliye Mkamilifu*

5 [c]"Pandeni na kushuka katika mitaa
ya Yerusalemu,
tazameni pande zote na mtafakari,
tafuteni katika viwanja vyake.
Kama mtaweza kumpata hata mtu
mmoja tu
atendaye kwa uaminifu na
kutafuta kweli,
nitausamehe mji huu.
2 [d]Ingawa wanasema, 'Kwa hakika
kama BWANA aishivyo,'
bado wanaapa kwa uongo."

3 [e]Ee BWANA, je, macho yako
hayaitafuti kweli?
Uliwapiga, lakini hawakusikia
maumivu,
uliwapondaponda, lakini
walikataa maonyo.
Walifanya nyuso zao kuwa ngumu
kuliko jiwe
nao walikataa kutubu.
4 [f]Ndipo nikasema, "Hawa ni maskini
tu;
wao ni wapumbavu,
kwa maana hawaijui njia ya BWANA,
sheria ya Mungu wao.
5 [g]Kwa hiyo nitakwenda kwa viongozi
na kuzungumza nao,
hakika wao wanaijua njia ya
BWANA,
sheria ya Mungu wao."
Lakini kwa nia moja nao pia
walikuwa wameivunja nira
na kuvivunja vifungo.
6 [h]Kwa hiyo simba kutoka mwituni
atawashambulia,
mbwa mwitu kutoka jangwani
atawaangamiza,
chui atawavizia karibu na miji yao,
ili kumrarua vipande vipande
yeyote atakayethubutu kutoka
nje,
kwa maana maasi yao ni makubwa,
na kukengeuka kwao kumekuwa
ni kwingi.

7 [i]"Kwa nini niwasamehe?
Watoto wenu wameniacha na
kuapa kwa miungu ambayo si
miungu.
Niliwapatia mahitaji yao yote,
lakini bado wamefanya uzinzi na
kusongana katika nyumba za
makahaba.
8 [j]Wamelishwa vizuri, kama farasi
waume wenye tamaa nyingi,
kila mmoja akimlilia mke wa
mwanaume mwingine.
9 [k]Je, nisiwaadhibu kwa ajili ya hili?"
asema BWANA.

---

[a]**4:30** Isa 10:3-4; Eze 16:11; 23:40; 2Fal 9:30; Ay 19:14; Eze 23:9; Za 35:4
[b]**4:31** Mwa 3:16; Mik 4:10; Isa 42:14; Mao 1:17; Yer 6:24; 13:21; 22:23; Za 9:14; Isa 42:14; Kum 32:25; Mao 2:21
[c]**5:1** Eze 22:30; Mwa 18:24; Mik 7:2; Yer 2:29; 2Nya 16:9; Za 45:10
[d]**5:2** Tit 1:16; Yer 4:2; Law 19:12
[e]**5:3** 2Nya 16:9; Yer 7:28; Isa 9:13; Sef 3:2; Zek 7:2; Eze 36:26; 3:8-9; Amo 4:6
[f]**5:4** Yer 8:7; Mit 10:21; Yer 4:22
[g]**5:5** Mik 3:1, 9; Za 2:3; Yer 2:20
[h]**5:6** Hos 13:7; Yer 4:7; 30:14; Za 7:12; Law 26:22
[i]**5:7** Yos 23:7; Yer 12:16; Gal 4:8; Amo 8:14; Kum 32:21; Hes 25:1; Yer 2:11; 13:27
[j]**5:8** Eze 22:11; 2Sam 11:2-4; Eze 33:26; Yer 29:23
[k]**5:9** Yer 44:22; Eze 7:9; Isa 1:24; 57:6

"Je, nisijilipizie kisasi
juu ya taifa kama hili?

10 [a]"Piteni katika mashamba yake ya
mizabibu na kuyaharibu,
lakini msiangamize kabisa.
Pogoeni matawi yake,
kwa kuwa watu hawa sio wa
BWANA.
11 [b]Nyumba ya Israeli na nyumba ya
Yuda
wamekuwa si waaminifu kwangu
kamwe,"
asema BWANA.

12 [c]Wamedanganya kuhusu BWANA.
Wamesema, "Yeye hatafanya
jambo lolote!
Hakuna dhara litakalotupata;
kamwe hatutaona upanga wala
njaa.
13 [d]Manabii ni upepo tu, wala neno
halimo ndani yao,
kwa hiyo hayo wayasemayo na
yatendeke kwao."

14 [e]Kwa hiyo hili ndilo asemalo BWANA Mungu Mwenye Nguvu Zote:

"Kwa sababu watu hawa wamesema
maneno haya,
nitayafanya maneno yangu
vinywani mwenu kuwa moto,
na watu hawa wawe kuni
zinazoliwa na huo moto.
15 [f]Ee nyumba ya Israeli," asema
BWANA,
"Ninaleta taifa toka mbali dhidi
yako,
taifa la kale na linaloendelea
kudumu,
taifa ambalo lugha yao huijui,
wala msemo wao huwezi
kuuelewa.
16 [g]Podo zao ni kama kaburi lililo wazi,
wote ni mashujaa hodari wa vita.
17 [h]Watayaangamiza mazao yenu na
chakula chenu,
wataangamiza wana wenu na
mabinti zenu;
wataangamiza makundi yenu ya
kondoo na ya ng'ombe,
wataangamiza mizabibu yenu na
mitini yenu.
Kwa upanga wataangamiza
miji yenye maboma
mliyoitumainia.

18 "Hata hivyo katika siku hizo,
sitakuangamiza kabisa," asema BWANA.
19 [i]"Nao watu watakapouliza, 'Kwa nini
BWANA, Mungu wetu ametufanyia mambo
haya yote?' utawaambia, 'Kama vile
mlivyoniacha mimi na kutumikia miungu
migeni katika nchi yenu wenyewe, ndivyo
sasa mtakavyowatumikia wageni katika
nchi ambayo si yenu.'

20 "Itangazie nyumba ya Yakobo hili
na ulipigie mbiu katika Yuda:
21 [j]Sikieni hili, enyi watu wapumbavu,
msio na akili,
mlio na macho lakini hamwoni,
mlio na masikio lakini hamsikii:
22 [k]Je, haiwapasi kuniogopa mimi?"
asema BWANA.
"Je, haiwapasi kutetemeka mbele
zangu?
Niliufanya mchanga kuwa mpaka wa
bahari,
kizuizi cha milele ambacho
haiwezi kupita.
Mawimbi yanaweza kuumuka, lakini
hayawezi kuupita;
yanaweza kunguruma, lakini
hayawezi kuuvuka.

[a]**5:10** Yer 39:8; 4:27; Amo 9:8
[b]**5:11** 1Fal 19:10; Yer 3:20; Za 73:27; Isa 24:16
[c]**5:12** Yer 23:17; 2Nya 36:16; Yer 28:7; Isa 28:15; Yer 14:13
[d]**5:13** Yer 14:15; 2Nya 36:16; Ay 6:26
[e]**5:14** Hos 6:5; Yer 1:9; 23:9; Za 39:3
[f]**5:15** Kum 28:49; Isa 5:26; 2Fal 24:2; Isa 28:11; Mwa 11:7
[g]**5:16** Ay 39:23
[h]**5:17** Yer 30:16; Law 26:16; Yer 50:7-17; Kum 28:31-33; Yer 8:16; Hes 16:14; Hos 2:12
[i]**5:19** Kum 29:24-26; 4:28; Yer 15:4; 13:22; 1Fal 9; 9; Yer 16:13
[j]**5:21** Isa 6:10; Eze 12:2; Mdo 28:26; Isa 42:20; Mk 8:18; Kum 32:6; Yer 4:22; Hes 2:18
[k]**5:22** Kum 28:58; Ay 4:14; Isa 64:2; Za 46:3

23 [a]Lakini watu hawa wana mioyo ya
ukaidi na ya uasi,
wamegeukia mbali na kwenda
zao.
24 [b]Wao hawaambiani wenyewe,
'Sisi na tumwogope BWANA
Mungu wetu,
anayetupatia mvua za masika na za
vuli kwa majira yake,
anayetuhakikishia majuma ya
mavuno kwa utaratibu.'
25 Matendo yenu mabaya yamezuia
haya yote,
dhambi zenu zimewazuia msipate
mema.

26 [c]"Miongoni mwa watu wangu wamo
walio waovu
wanaovizia kama watu wanaotega
ndege,
na kama wale wanaoweka mitego
kuwakamata watu.
27 Kama vitundu vilivyojaa ndege,
nyumba zao zimejaa udanganyifu;
wamekuwa matajiri na wenye
nguvu,
28 [d]wamenenepa na kunawiri.
Matendo yao maovu hayana kikomo;
hawatetei mashauri ya yatima
wapate kushinda,
hawatetei haki za maskini.
29 Je, nisiwaadhibu kwa ajili ya hili?"
asema BWANA.
"Je, nisijilipizie kisasi
juu ya taifa kama hili?

30 [e]"Jambo la kutisha na kushtusha
limetokea katika nchi hii:
31 [f]Manabii wanatabiri uongo,
makuhani wanatawala kwa
mamlaka yao wenyewe,
nao watu wangu wanapenda hivyo.
Lakini mtafanya nini mwisho
wake?

*Yerusalemu Imezingirwa Na Jeshi*

6 [g]"Kimbieni kwa usalama wenu, enyi
watu wa Benyamini!
Kimbieni kutoka Yerusalemu!
Pigeni tarumbeta katika Tekoa!
Inueni ishara juu ya
Beth-Hakeremu!
Kwa kuwa maafa yanaonekana
yakitoka kaskazini,
na uharibifu wa kutisha.
2 [h]Nitamwangamiza Binti Sayuni,
aliye mzuri sana na mwororo.
3 [i]Wachungaji pamoja na makundi yao
watakuja dhidi yake;
watapiga mahema yao kumzunguka,
kila mmoja akichunga kundi lake
mwenyewe."

4 [j]"Jiandaeni kwa vita dhidi yake!
Inukeni tumshambulie mchana!
Lakini, ole wetu, mchana unaisha,
na vivuli vya jioni vinazidi kuwa
virefu.
5 Kwa hiyo inukeni, tufanye
mashambulizi usiku,
na kuharibu ngome zake!"

6 [k]Hivi ndivyo asemavyo BWANA Mwenye
Nguvu Zote:

"Kateni miti mjenge boma
kuzunguka Yerusalemu.
Mji huu ni lazima uadhibiwe,
umejazwa na uonevu.
7 [l]Kama vile kisima kinavyomwaga
maji yake,
ndivyo anavyomwaga uovu wake.

---

[a]**5:23** Kum 21:18; Za 14:3
[b]**5:24** Mt 5:45; Yoe 2:23; Mwa 8:22; Mdo 14:17; Kum 6:24; Yak 5:7
[c]**5:26** Za 10:8; Mit 1:11; Mt 7; 15; Mhu 9:12; Yer 9:8; Mik 7:2
[d]**5:28** Kum 32:15; Zek 7:10; Kut 22:21-24; Amo 5:12; Za 73:12; 82:3
[e]**5:30** Yer 18:13; Hos 6:10; Yer 23:14
[f]**5:31** Eze 13:6; Isa 30:10; Mik 2:11; Mao 4:13; Hos 9:5
[g]**6:1** Yos 18:28; Neh 3:14; Yer 4:6; Hes 10:7; Yer 4:21; 2Nya 11:6
[h]**6:2** Za 9:14; Mao 4:5
[i]**6:3** Yer 12:10; 2Fal 25:4; Lk 19:43
[j]**6:4** Yer 15:8; 22:7
[k]**6:6** Kum 20:19-20; 2Sam 20:15; Eze 26:6-8; Kum 28:33; Yer 25:38; Sef 3:1
[l]**6:7** Isa 58:4; Yer 20:8; Mik 7:2-3; Za 55:9-11

Ukatili na maangamizi yasikika
ndani yake,
ugonjwa wake na majeraha yake
viko mbele yangu daima.
8 [a]Pokea onyo, ee Yerusalemu,
la sivyo nitageukia mbali nawe
na kuifanya nchi yako kuwa ukiwa,
asiweze mtu kuishi ndani yake."

9 Hivi ndivyo asemavyo BWANA Mwenye Nguvu Zote:

"Wao na wayakusanye mabaki ya
Israeli
kwa uangalifu kama kwenye
mzabibu;
pitisha mkono wako kwenye matawi
tena,
kama yeye avunaye zabibu."

10 [b]Niseme na nani na kumpa onyo?
Ni nani atakayenisikiliza mimi?
Masikio yao yameziba,[c]
kwa hiyo hawawezi kusikia.
Neno la BWANA ni chukizo kwao,
hawalifurahii.
11 [d]Lakini nimejaa ghadhabu ya
BWANA,
nami siwezi kuizuia.

"Wamwagie watoto walioko
barabarani,
na juu ya vijana waume
waliokusanyika;
mume na mke watakumbwa pamoja
ndani yake,
hata nao wazee waliolemewa na
miaka.
12 [e]Nyumba zao zitapewa watu
wengine,
pamoja na mashamba yao na wake
zao,
nitakapounyoosha mkono wangu
dhidi ya wale waishio katika
nchi,"
asema BWANA.
13 [f]"Kuanzia aliye mdogo kabisa hadi
aliye mkubwa kabisa,
wote wana tamaa ya kupata faida
zaidi;
manabii na makuhani wanafanana,
wote wanafanya udanganyifu.
14 [g]Wanafunga majeraha ya watu
wangu
bila uangalifu.
Wanasema, 'Amani, amani,'
wakati hakuna amani.
15 [h]Je, wanaona aibu kwa ajili ya tabia
yao
inayochukiza mno?
Hapana, hawana aibu hata kidogo;
hawajui hata kuona haya.
Kwa hiyo wataanguka miongoni
mwa hao walioanguka,
watashushwa chini
nitakapowaadhibu,"
asema BWANA.

16 [i]Hivi ndivyo asemavyo BWANA:

"Simama kwenye njia panda
utazame,
ulizia mapito ya zamani,
ulizia wapi ilipo njia nzuri, uifuate
hiyo,
nanyi mtapata raha nafsini
mwenu.
Lakini ninyi mlisema, 'Hatutaipita
hiyo.'
17 [j]Niliweka walinzi juu yenu na
kusema,
'Sikieni sauti ya tarumbeta!'
Lakini mkasema, 'Hatutasikiliza.'

---

[a]**6:8** Eze 23:18; Hos 9:12
[b]**6:10** Kut 6:12; Yer 15:10-15; Mdo 7:51; Yer 20:8; 7:13; 35:15; Isa 42:20
[c]10 Masikio yameziba kwa Kiebrania ina maana kwamba masikio yao hayajatahiriwa.
[d]**6:11** Yer 7:20; Ay 32:20; 2Nya 36:17; Isa 40:30; Yer 15:17; Mao 2:21
[e]**6:12** Kum 28:30; Yer 8:10; Mik 2:4; Yer 43:6; Sef 1:4; Eze 6:14; Yer 43:6; 38:22
[f]**6:13** Isa 56:11; Yer 8:10; Mao 4:13; Yer 2:29
[g]**6:14** Eze 13:10; Isa 30:10; Yer 4; 10
[h]**6:15** Mik 3:7; Zek 13:7; Yer 3:3; 8:10-12; 2Nya 25:16; Yer 27:15
[i]**6:16** Yer 18:15; Lk 16:29; Yos 1:13; Mt 11:29; 1Fal 8:36; Isa 11:10
[j]**6:17** Yer 25:4; Isa 52:8; Eze 3:17; 33:4; Kut 20:18; Yer 11:7-8

18 [a]Kwa hiyo sikilizeni, enyi mataifa,
angalieni, enyi mashahidi,
lile litakalowatokea.
19 Sikia, ee nchi:
Ninaleta maafa juu ya watu hawa,
matunda ya mipango yao,
kwa sababu hawakusikiliza maneno yangu
na wameikataa sheria yangu.
20 [b]Unanifaa nini uvumba kutoka Sheba,
au udi wa harufu nzuri kutoka nchi ya mbali?
Sadaka zako za kuteketezwa hazikubaliki,
dhabihu zako hazinifurahishi mimi."

21 [c]Kwa hiyo hivi ndivyo asemavyo BWANA:

"Nitaweka vikwazo mbele ya watu hawa.
Baba na wana wao watajikwaa juu yake,
majirani na marafiki wataangamia."

22 [d]Hivi ndivyo asemavyo BWANA:

"Tazama, jeshi linakuja
kutoka nchi ya kaskazini,
taifa kubwa linaamshwa
kutoka miisho ya dunia.
23 [e]Wamejifunga pinde na mkuki,
ni wakatili na hawana huruma.
Wanatoa sauti kama bahari inayonguruma
wanapoendesha farasi zao.
Wanakuja kama watu waliojipanga tayari kwa vita
ili kukushambulia, ee Binti Sayuni."

24 [f]Tumesikia taarifa zao,
nayo mikono yetu imelegea.
Uchungu umetushika,
maumivu kama ya mwanamke katika utungu wa kuzaa.
25 [g]Usitoke kwenda mashambani
au kutembea barabarani,
kwa kuwa adui ana upanga,
na kuna vitisho kila upande.
26 [h]Enyi watu wangu, vaeni magunia
mjivingirishe kwenye majivu,
ombolezeni kwa kilio cha uchungu
kama amliliaye mwana pekee,
kwa maana ghafula
mharabu atatujia.

27 [i]"Nimekufanya wewe kuwa kitu cha kujaribu chuma,
nao watu wangu kama mawe yenye madini,
ili upate kuzijua na kuzijaribu njia zao.
28 [j]Wote ni waasi sugu,
wakienda huku na huko kusengenya.
Wao ni shaba na chuma,
wote wanatenda upotovu.
29 Mivuo inavuma kwa nguvu,
kinachoungua kwa huo moto ni risasi,
lakini pamoja na kusafisha kote huku ni bure;
waovu hawaondolewi.
30 [k]Wanaitwa fedha iliyokataliwa,
kwa sababu BWANA amewakataa."

### *Dini Za Uongo Hazina Maana*

7 Hili ndilo neno lililomjia Yeremia kutoka
kwa BWANA: 2 [l]"Simama kwenye lango
la nyumba ya BWANA, na huko upige mbiu
ya ujumbe huu:
" 'Sikieni neno la BWANA, enyi watu wote

[a]**6:18** Mit 1:31; Eze 20:13; Kum 4:26; Amo 2:4; Yer 22:29; Yos 23:15; Yer 11:11; 29:19
[b]**6:20** Kut 30:23; Isa 60:6; Amo 5:22; Za 50:8-10; Hos 8:13; Mik 6:6-8; Mwa 10:7
[c]**6:21** Isa 8:14; Ay 5:12; Yer 13:16; Law 26:37
[d]**6:22** Yer 4:6; Kum 28:49
[e]**6:23** Isa 5:30; 13:18; Yer 4:29; Za 18:4; 93:3; Isa 10:32
[f]**6:24** Za 48:6; Yer 4:19, 31; 50:41-43; Isa 13:7
[g]**6:25** Ay 15:21; Za 31:13; Amo 5:6; Yer 49:29
[h]**6:26** Yer 4:8; Ay 2:8; Yon 3:6; Zek 12:10; Mwa 12:16; Yer 25:34; Eze 27:30; Kut 12:23
[i]**6:27** Yer 9:7; Zek 13:9
[j]**6:28** Yer 5:23; Eze 22:18; Yer 9:4; Law 19:16
[k]**6:30** Za 53:5; Mao 5:22; Hos 9:17; Mit 17:3; Eze 22; 18; Yer 7:29
[l]**7:2** Yer 17:19; 19:2-3

wa Yuda mliokuja kupitia malango haya ili
kumwabudu BWANA. 3 [a]Hili ndilo asemalo
BWANA Mwenye Nguvu Zote, Mungu wa
Israeli: Tengenezeni njia zenu na matendo
yenu, nami nitawaacha mkae mahali hapa.
4 [b]Msitumainie maneno ya udanganyifu na
kusema, “Hili ni Hekalu la BWANA, Hekalu
la BWANA, Hekalu la BWANA!” 5 [c]Kama
kweli mkibadili njia zenu na matendo
yenu, mkatendeana haki kila mmoja na
mwenzake, 6 [d]kama msipomwonea mgeni,
yatima wala mjane, na kumwaga damu
isiyo na hatia mahali hapa, nanyi kama
msipofuata miungu mingine kwa madhara
yenu wenyewe, 7 [e]ndipo nitawaacha mkae
mahali hapa, katika nchi niliyowapa baba
zenu milele na milele. 8 Lakini tazama,
mnatumainia maneno ya udanganyifu
yasiyo na maana.

9 [f]“ ‘Je, mtaiba na kuua, mtazini na
kuapa kwa uongo, na kufukiza uvumba
kwa Baali, na kufuata miungu mingine
ambayo hamkuijua, 10 [g]kisha mje na
kusimama mbele yangu katika nyumba hii
inayoitwa kwa Jina langu, mkisema, “Tuko
salama.” Salama kwa kufanya mambo haya
yote ya kuchukiza? 11 [h]Je, nyumba hii,
iitwayo kwa Jina langu, imekuwa pango
la wanyang’anyi kwenu? Lakini nimekuwa
nikiona yanayotendeka! asema BWANA.

12 [i]“ ‘Nendeni sasa mahali pangu
palipokuwa huko Shilo, mahali ambapo
nilipafanya pa kwanza kuwa makao ya
Jina langu, nanyi mwone lile nililopafanyia
kwa ajili ya uovu wa watu wangu Israeli.
13 [j]Mlipokuwa mnafanya yote haya, asema
BWANA, nilisema nanyi tena na tena, lakini
hamkusikiliza; niliwaita, lakini hamkujibu.
14 Kwa hiyo, nililolifanyia Shilo, nitalifanya
sasa kwa nyumba hii iitwayo kwa Jina langu,
Hekalu mnalolitumainia, mahali nilipowapa
ninyi na baba zenu. 15 [k]Nitawafukuza mbele
yangu, kama nilivyowafanyia ndugu zenu,
watu wa Efraimu.’

16 [l]“Kwa hiyo usiombe kwa ajili ya
watu hawa, wala usinililie, na usifanye
maombi kwa ajili yao; usinisihi, kwa
sababu sitakusikiliza. 17 Je, huyaoni hayo
wanayoyatenda katika miji ya Yuda na
katika barabara za Yerusalemu? 18 [m]Watoto
wanakusanya kuni, baba zao wanawasha
moto, na wanawake wanakanda unga
na kuoka mikate kwa ajili ya Malkia wa
Mbinguni. Wanamimina sadaka za vinywaji
kwa miungu mingine ili kunikasirisha.
19 [n]Lakini je, mimi ndiye wanayenikasirisha?
asema BWANA. Je, hawajiumizi wenyewe
na kujiaibisha?

20 [o]“ ‘Kwa hiyo hivi ndivyo asemavyo
BWANA Mwenyezi: Hasira yangu na
ghadhabu yangu itamwagwa mahali hapa,
juu ya mwanadamu na mnyama, juu ya miti
ya shambani na juu ya matunda ya ardhini,
nayo itaungua pasipo kuzimwa.

21 [p]“ ‘Hivi ndivyo asemavyo BWANA
Mwenye Nguvu Zote, Mungu wa Israeli:
Endeleeni, ongezeni sadaka zenu za
kuteketezwa juu ya dhabihu zenu nyingine,
mle nyama hiyo wenyewe! 22 Kwa kuwa
nilipowaleta baba zenu kutoka Misri
na kusema nao, sikuwapa amri kuhusu
sadaka za kuteketezwa na dhabihu tu,

---

[a]**7:3** Yer 26:13; 35:13; 18:11
[b]**7:4** Yer 28:15; Mik 3:11; Ay 15:31
[c]**7:5** Kut 22:22; Law 25:17; Isa 1:17; Yer 26:13
[d]**7:6** 2Fal 21:16; Kum 8:19; Yer 22:3; Kut 20:3; Yer 5:28; Eze 22:7; Yer 2:34
[e]**7:7** Kum 4:40; Yos 1:16
[f]**7:9** Yer 11:13-17; Kut 20:3; Hos 2:13; Kut 20:13-15; Law 19:12; Zek 8:17; Yer 32:29
[g]**7:10** 2Fal 21:4-5; Eze 23:38-39; Yer 23:11; 32:34; Eze 33:25
[h]**7:11** Isa 56:7; Mt 21:13; Mk 11:17; Mwa 31:50; Amu 11:10; Hes 11:29; Lk 19:40; Yer 42:5
[i]**7:12** 1Sam 4:10; Yos 18:1; Za 78:60-64; 1Sam 2:32; Kut 40:2; Yos 18:10; Dan 9:18
[j]**7:13** 2Nya 36:15; Isa 65:12; Yer 35:17; Za 71:17; Isa 48:17; Yer 32:33; Mit 1:24
[k]**7:15** Mwa 4:14; Kut 33; 15; 2Fal 17:20; Za 78:67; Yer 23:39
[l]**7:16** Kut 32:10; Kum 9:14; Hes 23:19
[m]**7:18** Yer 44:17; 19:13; Kum 31:17; 1Fal 14:9; Isa 57:6
[n]**7:19** Ay 7:20; 1Kor 10:22; Yer 22:22; Kum 32:21; Yer 44:3; 9:19
[o]**7:20** Ay 40:11; Mao 2:3-5; Isa 30:15; Yer 42:18; 6:11-12; Mao 4:11; Eze 20:47-48
[p]**7:21** Isa 1:11; Amo 5:21-22; 1Sam 2:12-17; Hos 8:13; Yer 6:20; 7:22; Isa 43:23; 1Sam 15:22

23 [a]lakini niliwapa amri hii nikisema: Nitiini
mimi, nami nitakuwa Mungu wenu nanyi
mtakuwa watu wangu. Enendeni katika njia
zote ninazowaamuru ili mpate kufanikiwa.
24 Lakini hawakusikiliza wala kujali. Badala
yake, walifuata ukaidi wa mioyo yao miovu.
Walirudi nyuma badala ya kusonga mbele.
25 [b]Tangu wakati ule baba zenu walipotoka
Misri hadi sasa, siku baada ya siku, tena
na tena nimewatumia watumishi wangu
manabii. 26 [c]Lakini hawakunisikiliza wala
hawakujali. Walikuwa na shingo ngumu na
kufanya maovu kuliko baba zao.’
27 [d]“Utakapowaambia haya yote,
hawatakusikiliza; utakapowaita,
hawatajibu. 28 Kwa hiyo waambie, ‘Hili ni
taifa ambalo halimtii BWANA, Mungu wao,
wala kukubali maonyo. Kweli imekufa,
imetoweka midomoni mwao. 29 [e]Nyoeni
nywele zenu na kuzitupa, ombolezeni
katika miinuko iliyo kame, kwa kuwa
BWANA amekikataa na kukiacha kizazi hiki
kilichomkasirisha.

*Bonde La Machinjo*

30 [f]“ ‘Watu wa Yuda wamefanya
maovu machoni pangu, asema BWANA.
Wameziweka sanamu zao za machukizo
ndani ya nyumba iitwayo kwa Jina langu, na
wameitia unajisi. 31 [g]Wamejenga mahali pa
juu pa kuabudia sanamu pa Tofethi kwenye
Bonde la Ben-Hinomu ili kuwateketeza
wana wao na binti zao kwenye moto, kitu
ambacho sikuamuru, wala hakikuingia
akilini mwangu. 32 [h]Kwa hiyo mjihadhari,
siku zinakuja, asema BWANA, wakati watu
watakapokuwa hawapaiti Tofethi au Bonde
la Ben-Hinomu, lakini watapaita Bonde la
Machinjo, kwa sababu watawazika wafu
huko Tofethi mpaka pasiwe tena nafasi.
33 [i]Ndipo mizoga ya watu hawa itakuwa
chakula cha ndege wa angani na wanyama
wa nchi, wala hapatakuwepo na yeyote
wa kuwafukuza. 34 [j]Nitazikomesha sauti
za shangwe na furaha, na sauti za bwana
arusi na bibi arusi katikati ya miji ya Yuda
na barabara za Yerusalemu, kwa sababu
nchi itakuwa ukiwa.

8 [k]“ ‘Wakati huo, asema BWANA, mifupa
ya wafalme na maafisa wa Yuda, mifupa
ya makuhani na manabii, na mifupa ya
watu wa Yerusalemu itaondolewa kutoka
makaburi yao. 2 [l]Itawekwa wazi kwa
jua, na mwezi, na nyota zote za mbingu,
ambazo walizipenda na kuzitumikia, na
ambazo wamezifuata kutafuta ushauri
na kuziabudu. Hawatakusanywa pamoja
au kuzikwa, lakini watakuwa kama mavi
yaliyotapakaa juu ya ardhi. 3 [m]Popote
nitakapowafukuzia, mabaki wote wa kizazi
hiki kiovu watatamani kufa kuliko kuishi,
asema BWANA Mwenye Nguvu Zote.’

*Dhambi Na Adhabu*

4 [n]“Waambie, ‘Hivi ndivyo asemavyo
BWANA:

“ ‘Je, watu wanapoanguka
hawainuki?
Je, mtu anapopotea harudi?
5 [o]Kwa nini basi watu hawa walipotea?
Kwa nini Yerusalemu inapotea kila
mara?
Wanang’ang’ania udanganyifu
na wanakataa kurudi.

[a]**7:23** Kut 15:26; 19:5; Law 26:12; Kum 5:33; 1Yn 3:23; Isa 51:16; 1Fal 8:36; 7:24; Za 81:11-12; Kum 29:19; Yer 34:14; 6:10; 11:8; 17:23; 3:17; 2:19
[b]**7:25** Neh 9:30; Yer 25:4; 2Nya 36:15; Isa 20:3; Hes 11:29; Yer 35:15
[c]**7:26** Za 81:11; Kut 32:9; Mdo 7:51; Yer 16:12; Lk 11:27
[d]**7:27** Eze 2:7; Zek 7:13; Eze 3:7; Isa 65:12
[e]**7:29** Isa 15:2; Hos 11:8; Mik 5:3; Law 21:5; Ay 1:20; Yer 4:8; 6:30; 12:7
[f]**7:30** Yer 2:7; 32:34; Eze 7:20-22; Law 20:3
[g]**7:31** 2Fal 23:10; Law 18:21; Za 106:38; Eze 20:31; Mik 6:7; Yos 15:8; 2Nya 33:6
[h]**7:32** Yer 19:6; 19:11
[i]**7:33** Kum 28:26; Eze 29:5; Mwa 15:11; Yer 6:11; 14:16
[j]**7:34** Hos 2:11; Isa 24:8; Eze 26:13; Ufu 18:23; Zek 7:14; Mt 23:38; Isa 24:7-12
[k]**8:1** Isa 14:19; Za 53:5
[l]**8:2** Yer 44:19; Mdo 7:42; Za 83:10; 2Fal 23:5; Yer 19:13; Ay 31:27; Yer 14:16
[m]**8:3** Ay 3:22; Ufu 9:6; Kum 29:28
[n]**8:4** Mik 7:8; Mit 24:16; Yer 31:19; Za 119:67
[o]**8:5** Yer 5:27; Isa 1:20; Yer 7:24; Zek 7:11

6 [a]Nimewasikiliza kwa makini,
lakini hawataki kusema lililo sawa.
Hakuna anayetubia makosa yake
akisema, "Nimefanya nini?"
Kila mmoja hufuata njia yake mwenyewe
kama farasi anayekwenda vitani.
7 [b]Hata korongo aliyeko angani
anayajua majira yake yaliyoamriwa,
nao njiwa, mbayuwayu na koikoi
hufuata majira yao ya kurudi.
Lakini watu wangu hawajui
BWANA anachotaka kwao.

8 [c]" 'Mwawezaje kusema, "Sisi tuna busara
kwa sababu tunayo sheria ya BWANA,"
wakati ambapo kwa hakika kalamu ya uongo ya waandishi
imeandika kwa udanganyifu?
9 [d]Wenye hekima wataaibika,
watafadhaika na kunaswa.
Kwa kuwa wamelikataa neno la BWANA,
hiyo hekima waliyo nayo ni ya namna gani?
10 [e]Kwa hiyo nitawapa watu wengine wake zao,
na mashamba yao kwa wamiliki wengine.
Kuanzia aliye mdogo kabisa hadi aliye mkubwa kabisa,
wote wana tamaa ya kupata zaidi;
manabii na makuhani wanafanana,
wote wanafanya udanganyifu.
11 [f]Wanafunga majeraha ya watu wangu
bila uangalifu.
Wanasema, "Amani, amani,"
wakati hakuna amani.
12 [g]Je, wanaona aibu kwa ajili ya tabia yao inayochukiza mno?
Hapana, hawana aibu hata kidogo,
hawajui hata kuona haya.
Kwa hiyo wataanguka miongoni mwa hao walioanguka,
watashushwa chini watakapoadhibiwa,
asema BWANA.

13 [h]" 'Nitayaondoa mavuno yao,
asema BWANA.
Hapatakuwepo zabibu kwenye mzabibu.
Hapatakuwepo na tini kwenye mtini,
majani yake yatanyauka.
Kile nilichowapa watanyang'anywa.' "

14 [i]"Kwa nini tunaketi hapa?
Kusanyikeni pamoja!
Tukimbilie kwenye miji yenye maboma,
tukaangamie huko!
Kwa kuwa BWANA, Mungu wetu
ametuhukumu kuangamia,
na kutupa maji yenye sumu tunywe,
kwa sababu tumemtenda dhambi.
15 [j]Tulitegemea amani,
lakini hakuna jema lililokuja,
tulitegemea wakati wa kupona,
lakini kulikuwa hofu tu.
16 [k]Mkoromo wa farasi za adui
umesikika kuanzia Dani,
kwa mlio wa madume yao ya farasi,
nchi yote inatetemeka.
Wamekuja kuangamiza nchi na vyote vilivyomo,
mji na wote waishio ndani yake."

17 [l]"Tazama, nitatuma nyoka wenye sumu kali katikati yenu,
fira ambao hawawezi kulogwa,
nao watawauma,"
asema BWANA.

[a]**8:6** 2Pet 3:9; Ufu 9:20; Za 14:1-3; Mal 3:16
[b]**8:7** Kum 32:28; Wim 2:12; Yer 4:22
[c]**8:8** Rum 2:17; Hos 8:12
[d]**8:9** Isa 29:14; Yer 5:16-19; 2Fal 19:26; Ay 5:13; Yer 6:19; 1Kor 1:20
[e]**8:10** Yer 6:12; Isa 56:11; Mao 4:13; Isa 28:7; Yer 14:14; Mao 2:14; Yer 23:11-15
[f]**8:11** Yer 6:14; Eze 13:10; 7:25; Yer 4:10
[g]**8:12** Za 52:5-7; Yer 3:3; Isa 3:9; Yer 6:15
[h]**8:13** Hos 2:12; Mt 21:19; Yer 5:17; Lk 13:6
[i]**8:14** Yos 10:20; Yer 23:15; Kum 29:18; Dan 9:5; Yer 35:11; 9:15; 14:7, 20
[j]**8:15** Ay 19:8; Yer 14:19
[k]**8:16** Mwa 30:6; Yer 4:15, 29; 51:29; 5:17
[l]**8:17** Hes 21:6; Kum 32:24; Isa 3:3; Za 58:5

18 [a]Ee Mfariji wangu katika huzuni,
moyo wangu umezimia ndani yangu.
19 [b]Sikia kilio cha watu wangu
kutoka nchi ya mbali:
"Je, BWANA hayuko Sayuni?
Je, Mfalme wake hayuko tena huko?"

"Kwa nini wamenikasirisha kwa vinyago vyao,
kwa sanamu zao za kigeni zisizofaa?"

20 "Mavuno yamepita,
kiangazi kimekwisha,
nasi hatujaokolewa."

21 [c]Kwa kuwa watu wangu wamepondwa, nami nimepondeka pia;
ninaomboleza, nayo hofu kuu imenishika.
22 [d]Je, hakuna zeri ya kuponya katika Gileadi?
Je, hakuna tabibu huko?
Kwa nini basi hakuna uponyaji
wa majeraha ya watu wangu?

9

1 [e]Laiti kichwa changu kingekuwa chemchemi ya maji
na macho yangu yangekuwa kisima cha machozi!
Ningelia usiku na mchana
kwa kuuawa kwa watu wangu.
2 [f]Laiti ningekuwa na nyumba
ya kukaa wasafiri jangwani,
ningewaacha watu wangu
na kwenda mbali nao,
kwa kuwa wote ni wazinzi,
kundi la watu wadanganyifu.

3 [g]"Huweka tayari ndimi zao kama upinde,
ili kurusha uongo;
wamekuwa na nguvu katika nchi
lakini si katika ukweli.
Wanatoka dhambi moja hadi nyingine,
hawanitambui mimi,"
asema BWANA.
4 [h]"Jihadhari na rafiki zako;
usiwaamini ndugu zako.
Kwa kuwa kila ndugu ni mdanganyifu,
na kila rafiki ni msingiziaji.
5 [i]Rafiki humdanganya rafiki,
hakuna yeyote asemaye kweli.
Wamefundisha ndimi zao kudanganya,
wanajichosha wenyewe katika kutenda dhambi.
6 [j]Unakaa katikati ya udanganyifu;
katika udanganyifu wao wanakataa kunitambua mimi,"
asema BWANA.

7 [k]Kwa hiyo hili ndilo asemalo BWANA
Mwenye Nguvu Zote:

"Tazama, nitawasafisha na kuwajaribu,
kwani ni nini kingine niwezacho kufanya
kwa sababu ya dhambi ya watu wangu?
8 [l]Ndimi zao ni mshale wenye sumu,
hunena kwa udanganyifu.
Kwa kinywa chake kila mmoja huzungumza maneno mazuri na jirani yake,
lakini moyoni mwake humtegea mtego.

[a]**8:18** Mao 5:17
[b]**8:19** Kum 28:64; Yer 9:16; Mik 4:9; Yer 44:3; Isa 41:24; Kum 32:21
[c]**8:21** Nah 2:10; Mao 2:13; Eze 6:9; Za 94:5; Isa 43:24; Yer 4:19
[d]**8:22** Mwa 37:25; Yer 30:12; Ay 13:4; Isa 1:6
[e]**9:1** Mao 3:48; Isa 22:4; Za 119:136; Yer 13:17; 14:17; Mao 2:11
[f]**9:2** Hes 25:1; Hos 4:2; Za 55:7; Yer 23:10; Hos 7:4; 1Fal 19:10; Isa 24:16
[g]**9:3** Kut 20:16; Mik 6:12; Amu 2:10; 1Sam 2:12; Za 64:3; Isa 44; 20; Yer 18:18
[h]**9:4** Mik 7:5-6; Mwa 27:35; 2Sam 15:12; Kut 20:16; Law 19:16
[i]**9:5** Za 15:2; Law 6:2; Isa 59:15
[j]**9:6** Yer 5:27; Mit 1:24
[k]**9:7** Ay 28:1; Isa 1:28; Hos 11:8; Yer 6:27
[l]**9:8** Za 35:20; Yer 5:26; Isa 3:5

9 [a]Je, nisiwaadhibu kwa ajili ya jambo hili?"
asema BWANA.
"Je, nisijilipizie kisasi
kwa taifa kama hili?"

10 [b]Nitalia na kuomboleza kwa ajili ya milima
na kuomboleza kuhusu malisho ya jangwani.
Yamekuwa ukiwa, wala hakuna apitaye humo,
milio ya ng'ombe haisikiki.
Ndege wa angani wametoroka
na wanyama wamekimbia.

11 [c]"Nitaifanya Yerusalemu lundo la magofu,
makao ya mbweha;
nami nitaifanya miji ya Yuda kuwa ukiwa
ili asiwepo atakayeishi humo."

12 [d]Ni mtu yupi aliye na hekima ya kutosha
ayaelewe haya? Ni nani aliyefundishwa na
BWANA awezaye kuyaeleza haya? Kwa nini
nchi imeharibiwa na kufanywa ukiwa kama
jangwa ambapo hakuna awezaye kupita?
13 [e]BWANA akasema, "Ni kwa sababu
wameiacha sheria yangu, niliyoiweka mbele
yao: hawajaniheshimu mimi wala kufuata
sheria yangu. 14 [f]Badala yake wamefuata
ukaidi wa mioyo yao, wamefuata Mabaali,
kama vile baba zao walivyowafundisha."
15 [g]Kwa hiyo, hivi ndivyo asemavyo BWANA
Mwenye Nguvu Zote, Mungu wa Israeli:
"Tazama, nitawafanya watu hawa wale
chakula kichungu na kunywa maji yenye
sumu. 16 [h]Nitawatawanya katika mataifa
ambayo wao wala baba zao hawakuwajua,
nikiwafuata kwa upanga mpaka niwe
nimewaangamiza kabisa."

17 [i]Hivi ndivyo asemavyo BWANA Mwenye Nguvu Zote:

"Fikiri sasa! Waite wanawake
waombolezao waje,
waite wale walio na ustadi kuliko wote.
18 [j]Nao waje upesi
na kutuombolezea,
mpaka macho yetu yafurike machozi
na vijito vya maji vitoke kwenye kope zetu.
19 [k]Sauti ya kuomboleza imesikika kutoka Sayuni:
'Tazama jinsi tulivyoangamizwa!
Tazama jinsi aibu yetu ilivyo kubwa!
Ni lazima tuihame nchi yetu
kwa sababu nyumba zetu zimekuwa magofu.' "

20 [l]Basi, enyi wanawake, sikieni neno la BWANA;
fungueni masikio yenu msikie
maneno ya kinywa chake.
Wafundisheni binti zenu kuomboleza;
fundishaneni kila mmoja na
mwenzake maombolezo.
21 [m]Mauti imeingia ndani kupitia madirishani,
imeingia kwenye majumba yetu ya fahari;
imewakatilia mbali watoto katika barabara
na vijana waume kutoka viwanja vya miji.

22 [n]Sema, "Hili ndilo asemalo BWANA:

" 'Maiti za wanaume zitalala
kama mavi katika mashamba,

---

[a]**9:9** Kum 32:43; Isa 10:3
[b]**9:10** Hos 4:3; Yoe 1:18; Yer 31:35; 32:18; 23:10; 4:25; 12:4
[c]**9:11** Ay 30:29; Isa 34:13; Law 26:31; Mao 1:4; Yer 26:18; Isa 25:2
[d]**9:12** Za 107:43; Hos 14:9
[e]**9:13** 2Nya 7:19; Za 89:30-32
[f]**9:14** Amo 2:4; Yer 3:17; 7:24; 2:8
[g]**9:15** Mao 3:15; Yer 8:14; Za 80:5
[h]**9:16** Law 26:33; Kum 28:64; 4:32; Eze 5:12; Yer 44:27; 8:19
[i]**9:17** 2Nya 35:25; Amo 5:15-16; Mhu 12:5
[j]**9:18** Za 119:136; Mao 3:48; Yer 14:17
[k]**9:19** Law 18:29; Yer 4:13
[l]**9:20** Isa 32:9-13; Yer 23:16
[m]**9:21** 2Nya 36:17; Isa 40:30; Yoe 2:9; Yer 16:6
[n]**9:22** 2Fal 9:37; Yer 8:2

kama malundo ya nafaka nyuma ya mvunaji,
wala hakuna anayekusanya.' "

23 [a]Hili ndilo asemalo BWANA:

"Mwenye hekima asijisifu katika hekima yake,
au mwenye nguvu ajisifu katika nguvu zake,
wala tajiri ajisifu katika utajiri wake,
24 [b]lakini yeye ajisifuye, na ajisifu kwa sababu hili:
kwamba ananifahamu na kunijua mimi,
kwamba mimi ndimi BWANA, nitendaye wema,
hukumu na haki duniani,
kwa kuwa napendezwa na haya,"
asema BWANA.

25 [c]"Siku zinakuja, nitakapowaadhibu
wale wote ambao wametahiriwa kimwili
tu, asema BWANA, 26 [d]yaani Misri, Yuda,
Edomu, Amoni, Moabu na wote wanaoishi
jangwani sehemu za mbali. Kwa maana
mataifa haya yote hayakutahiriwa
mioyo yao, nayo nyumba yote ya Israeli
haikutahiriwa."

*Mungu Na Sanamu*

10 Sikieni lile ambalo BWANA, anena
nanyi ee nyumba ya Israeli. 2 [e]Hili
ndilo asemalo BWANA:

"Usijifunze njia za mataifa
wala usitishwe na ishara katika anga,
ingawa mataifa yanatishwa nazo.
3 [f]Kwa maana desturi za mataifa hazina maana,
wanakata mti msituni,
na fundi anauchonga kwa patasi.
4 [g]Wanaparemba kwa fedha na dhahabu,
wanakikaza kwa nyundo na misumari ili kisitikisike.
5 [h]Sanamu zao ni kama sanamu
iliyowekwa shambani la matango kutishia ndege
nazo haziwezi kuongea;
sharti zibebwe
sababu haziwezi kutembea.
Usiziogope; haziwezi kudhuru,
wala kutenda lolote jema."

6 [i]Hakuna aliye kama wewe, Ee BWANA;
wewe ni mkuu,
jina lako ni lenye nguvu katika uweza.
7 [j]Ni nani ambaye haimpasi kukuheshimu wewe,
Ee Mfalme wa mataifa?
Hii ni stahili yako.
Miongoni mwa watu wote wenye hekima
katika mataifa na katika falme zao zote,
hakuna aliye kama wewe.
8 [k]Wote hawana akili, tena ni wapumbavu,
wanafundishwa na sanamu za miti zisizofaa lolote.
9 [l]Huleta fedha iliyofuliwa kutoka Tarshishi
na dhahabu kutoka Ufazi.

[a]**9:23** Ay 4:12; Isa 5:21; Mhu 9:11; Za 62:10; 1Fal 20:11; Mit 11:28; Eze 28:4-5; Yer 48:7
[b]**9:24** Gal 6:14; 2Kor 10:17; Za 34:2; Mik 6:8; Za 36:6; 1Kor 1:31
[c]**9:25** Law 26:41; Rum 2:8-9; Amo 3:2
[d]**9:26** Yer 25:23; 49:32; Mdo 7:51; Rum 2:28; Eze 31:18; 1Sam 14:6
[e]**10:2** Kut 23:24; Law 20:23; Mwa 1:14
[f]**10:3** Isa 40:19; Kum 9:21; Eze 7:20; Yer 44:8; 1Fal 8:36
[g]**10:4** 1Sam 5:3; Isa 41:7; Za 135:15; Hos 13:2; Hab 2:19
[h]**10:5** 1Fal 18:26; 1Kor 12:2; Isa 45:20; Hab 2:19; Isa 44:9-20; Mdo 19:26
[i]**10:6** 2Sam 7:22; Kut 8:9-10; Za 48:1
[j]**10:7** Isa 12:4; Ufu 15:4; Za 22:28; Yer 5:22
[k]**10:8** Isa 40:19; Yer 4:22; Isa 44:18; Kum 32:21
[l]**10:9** Dan 10:5; Za 115:4; Isa 40:19; Mwa 10:4

Kile ambacho fundi na sonara
wametengeneza
huvikwa mavazi ya rangi ya
samawi na urujuani:
vyote vikiwa vimetengenezwa
na mafundi stadi.
10 [a]Lakini BWANA ni Mungu wa kweli,
yeye ndiye Mungu aliye hai,
Mfalme wa milele.
Anapokasirika, dunia hutetemeka,
mataifa hayawezi kustahimili
hasira yake.

11 [b]"Waambie hivi: 'Miungu hii, ambayo
haikuumba mbingu na dunia, itaangamia
kutoka dunia na kutoka chini ya mbingu.' "

12 [c]Lakini Mungu aliiumba dunia kwa
uweza wake,
akaweka misingi ya ulimwengu
kwa hekima yake,
na akazitandaza mbingu kwa
ufahamu wake.
13 [d]Atoapo sauti yake, maji yaliyo
katika mbingu hunguruma;
huyafanya mawingu yainuke
kutoka miisho ya dunia.
Hupeleka umeme wa radi pamoja na
mvua,
naye huuleta upepo kutoka ghala
zake.

14 Kila mmoja ni mjinga na hana
maarifa,
kila sonara ameaibishwa na
sanamu zake.
Vinyago vyake ni vya udanganyifu,
havina pumzi ndani yavyo.
15 [e]Havifai kitu, ni vitu vya kufanyia
mzaha tu,
hukumu yavyo itakapowadia,
vitaangamia.
16 [f]Yeye aliye Fungu la Yakobo sivyo
alivyo,
kwani ndiye Muumba wa vitu
vyote,
pamoja na Israeli, kabila la urithi
wake:
BWANA Mwenye Nguvu Zote ndilo
jina lake.

*Maangamizi Yajayo*

17 [g]Kusanyeni mali na vitu vyenu
mwondoke nchi hii,
enyi mnaoishi katika hali ya
kuzingirwa na jeshi.
18 [h]Kwa kuwa hili ndilo asemalo
BWANA:
"Wakati huu, nitawatupa nje kwa
nguvu
wote waishio katika nchi hii;
nitawataabisha
ili waweze kutekwa."

19 [i]Ole wangu mimi kwa ajili ya
kuumia kwangu!
Jeraha langu ni kubwa!
Lakini nilisema,
"Kweli hii ni adhabu yangu,
nami sharti niistahimili."
20 [j]Hema langu limeangamizwa;
kamba zake zote zimekatwa.
Wana wangu wametekwa na hawapo
tena;
hakuna hata mmoja aliyebaki wa
kusimamisha hema langu
wala wa kusimamisha kibanda
changu.
21 [k]Wachungaji hawana akili
wala hawamuulizi BWANA,
hivyo hawastawi
na kundi lao lote la kondoo
limetawanyika.

[a]**10:10** 1Tim 6:17; Za 76:7; Yos 3:10; Mt 16:16; Mwa 21:33; Dan 6:26; Amu 5:4; Ay 9:6
[b]**10:11** Za 96:5; Isa 2:18
[c]**10:12** Ay 9:9; 38:4; Isa 40:22-28; Mdo 14:15; 1Sam 2:8; Mwa 1:1, 8, 31
[d]**10:13** Ay 36:29; Za 135:7; 104:13; Kum 28:12
[e]**10:15** Isa 41:21; Yer 14; 22
[f]**10:16** Kum 32:9; Yer 32:17; Kut 34:9; Za 73:26; Yer 31:35; Za 74:2
[g]**10:17** Eze 12:12
[h]**10:18** 1Sam 25:29; Isa 22:17; Eze 6:10; Kum 28:52
[i]**10:19** Mik 7:9; Nah 3:19; Ay 34:6; Yer 14:17; 15:18; Mao 2:13; Yer 30:12, 15
[j]**10:20** Yer 4:20; 31:15; Mao 1:5
[k]**10:21** Yer 23:2; Eze 34:6; Yer 6:22; 25:34; 50:6; Isa 56:10; Yer 22:30

22 [a]Sikilizeni! Taarifa inakuja:
ghasia kubwa kutoka nchi ya
kaskazini!
Hii itafanya miji ya Yuda ukiwa,
makao ya mbweha.

*Maombi Ya Yeremia*

23 [b]Ninajua, Ee BWANA, kwamba
maisha ya mwanadamu si
yake mwenyewe;
hawezi kuziongoza hatua zake
mwenyewe.
24 [c]Unirudi, Ee BWANA, lakini kwa
kipimo cha haki:
si katika hasira yako,
usije ukaniangamiza.
25 [d]Umwage ghadhabu yako juu ya
mataifa
wasiokujua wewe,
juu ya mataifa wasioliitia jina
lako.
Kwa kuwa wamemwangamiza
Yakobo;
wamemwangamiza kabisa
na kuiharibu nchi yake.

*Agano Limevunjwa*

11 Hili ndilo neno lililomjia Yeremia
kutoka kwa BWANA: 2 "Sikia maneno ya
agano hili, nawe uwaambie watu wa Yuda
na wale waishio Yerusalemu. 3 [e]Waambie
kwamba hili ndilo asemalo BWANA, Mungu
wa Israeli: 'Amelaaniwa mtu ambaye
hatayatii maneno ya agano hili, 4 [f]maneno
niliyowaamuru baba zenu nilipowatoa
katika nchi ya Misri, kutoka tanuru la
kuyeyushia vyuma.' Nilisema, 'Nitiini mimi
na mfanye kila kitu ninachowaamuru, nanyi
mtakuwa watu wangu, nami nitakuwa
Mungu wenu. 5 [g]Kisha nitatimiza kiapo
nilichowaapia baba zenu, kuwapa nchi
itiririkayo maziwa na asali,' nchi ambayo
mnaimiliki leo."
Nikajibu, "Amen, BWANA."
6 [h]BWANA akaniambia, "Tangaza maneno
haya yote katika miji ya Yuda na katika
barabara za Yerusalemu: 'Sikilizeni maneno
ya agano hili na kuyafuata. 7 [i]Tangu
wakati ule niliwapandisha baba zenu
kutoka Misri mpaka leo, niliwaonya tena
na tena, nikisema "Nitiini mimi." 8 [j]Lakini
hawakusikiliza wala kujali. Badala yake,
walifuata ukaidi wa mioyo yao miovu.
Hivyo nikaleta juu yao laana zote za agano
nililokuwa nimewaamuru wao kulifuata,
lakini wao hawakulishika.' "
9 [k]Kisha BWANA akaniambia, "Kuna
shauri baya linaloendelea miongoni
mwa watu wa Yuda na wale wanaoishi
Yerusalemu. 10 [l]Wamerudia dhambi za baba
zao, waliokataa kusikiliza maneno yangu.
Wameifuata miungu mingine kuitumikia.
Nyumba zote mbili za Israeli na Yuda
zimelivunja agano nililofanya na baba zao.
11 [m]Kwa hivyo, hili ndilo asemalo BWANA:
'Nitaleta juu yao maafa ambayo hawawezi
kuyakimbia. Hata kama wakinililia,
sitawasikiliza. 12 [n]Miji ya Yuda na watu
wa Yerusalemu watakwenda kuililia
miungu ambayo wameifukizia uvumba,
lakini haitawasaidia kamwe wakati maafa
yatakapowapiga. 13 [o]Mnayo miungu mingi
kama miji mliyo nayo, ee Yuda, nazo
madhabahu mlizozijenga za kufukizia

[a]**10:22** Isa 34:13; Yer 9:11; 6:22; 27:6; Eze 12:19
[b]**10:23** Ay 33:29; Yer 9:11; 6:22; 27:6; Eze 12:19
[c]**10:24** Yer 7:20; 18:23; 46:28; 30:11
[d]**10:25** Ay 15:21; Yer 8:16; Za 69:24; 79:6-7; Sef 3:8; Yer 2:3
[e]**11:3** Kum 11:26-28; 27:26; Gal 3:10; Kum 28:15-68
[f]**11:4** Law 26:3; Kum 4:20; 1Fal 8:51; Kut 24:8; Yer 7:23; Eze 11:20
[g]**11:5** Kum 7:12; Kut 6:8; 13:5; Za 105:8-11; Kut 3:8; Kum 27:26
[h]**11:6** Kut 15:26; Yn 13:17; Rum 2:13; Yak 1:22; Yer 4:5; Kum 15:5
[i]**11:7** 2Nya 36:15
[j]**11:8** Yer 7:26; Law 26:14-43; Yos 23:15; Mhu 9:3; Yer 3:17; 2Nya 7:19; Za 78:10
[k]**11:9** Hos 6:9; Eze 1:28; 22:25
[l]**11:10** Eze 20:18; Kum 9:7; 2Nya 30:7; Amu 2:11-13; 10:13; Zek 7:11; Yer 16:11; 34:18
[m]**11:11** Eze 8:8-18; Ay 27:9; Za 66:18; 2Fal 22:16; Zek 7:13; Ay 11:20; Yer 14:12
[n]**11:12** Kum 32:37-38; Amu 10:14; Yer 44:17; Isa 45:20
[o]**11:13** Yer 44:21; 3:24; Kut 20:3; Yer 19:4; 2Fal 17:29; Yer 7:9

uvumba huyo mungu wa aibu Baali ni nyingi kama barabara za Yerusalemu.'
14 [a]"Wewe usiwaombee watu hawa wala kufanya maombezi yoyote au kunisihi kwa ajili yao, kwa sababu sitawasikiliza watakaponiita wakati wa taabu yao.

15 [b]"Mpenzi wangu anafanya nini
hekaluni mwangu,
anapofanya mashauri yake maovu
na wengi?
Je, nyama iliyowekwa wakfu yaweza
kuondolea mbali adhabu yako?
Unapojiingiza katika ubaya wako,
ndipo unashangilia."

16 [c]BWANA alikuita mti wa mzeituni
uliostawi
ulio na matunda mazuri kwa sura.
Lakini kwa ngurumo ya mawimbi
makuu
atautia moto,
nayo matawi yake yatavunjika.

17 [d]BWANA Mwenye Nguvu Zote, aliyekupanda, ametamka maafa kwa ajili yako, kwa sababu nyumba ya Israeli na nyumba ya Yuda mmefanya maovu na kunikasirisha kwa kumfukizia Baali uvumba.

*Shauri Baya Dhidi Ya Yeremia*

18 Kwa sababu BWANA alinifunulia
hila zao mbaya, nilizifahamu, kwa kuwa
wakati ule alinionyesha yale waliyokuwa
wanayafanya. 19 [e]Nilikuwa kama mwana-
kondoo mpole aliyeongozwa machinjoni; mimi sikutambua kwamba walikuwa wamefanya shauri baya dhidi yangu, wakisema,

"Sisi na tuuangamize mti na
matunda yake;
nasi tumkatilie mbali kutoka nchi
ya walio hai,
ili jina lake lisikumbukwe tena."
20 [f]Lakini, Ee BWANA Mwenye Nguvu
Zote, wewe uhukumuye kwa
haki,
nawe uchunguzaye moyo na akili,
wacha nione ukiwalipiza wao kisasi,
kwa maana kwako nimeweka
shauri langu.

21 [g]"Kwa hiyo hili ndilo BWANA
asemalo kuhusu watu wa Anathothi wale wanaotafuta uhai wako wakisema, 'Usitoe unabii kwa jina la BWANA, la
sivyo utakufa kwa mikono yetu': 22 [h]kwa
hiyo hili ndilo BWANA Mwenye Nguvu Zote asemalo: 'Nitawaadhibu. Vijana wao waume watakufa kwa upanga, wana wao na
binti zao kwa njaa. 23 [i]Hawatasaziwa hata
mabaki kwao, kwa sababu nitaleta maafa kwa watu wa Anathothi katika mwaka wa adhabu yao.' "

*Lalamiko La Yeremia*

12 [j]Wewe daima u mwenye haki, Ee
BWANA,
niletapo mashtaka mbele yako.
Hata hivyo nitazungumza nawe
kuhusu hukumu yako:
Kwa nini njia ya waovu
inafanikiwa?
Kwa nini wasio waaminifu
wote wanaishi kwa raha?
2 [k]Umewapanda, nao wameota,
wanakua na kuzaa matunda.
Daima u midomoni mwao,
lakini mbali na mioyo yao.

[a]**11:14** Kut 32:10; Yer 7:16
[b]**11:15** Eze 16:25; Hag 2:12; Yer 7:9-10
[c]**11:16** Yer 7:20; 21:14; Rum 11:17-24; Hos 14:6; Isa 27:11
[d]**11:17** Kut 15:17; Isa 5:2; Yer 7:9; 12:2; 7:18
[e]**11:19** Za 54:3; Yer 20:10; Ay 28:13; Za 83:4; 44:22; Yer 18:18; Ay 28:13; Isa 53:8
[f]**11:20** Mdo 17:31; Za 7:8-9, 11; 1Sam 2:3; 1Nya 29:17; Za 58:10; Mao 3:60
[g]**11:21** Yer 12:6; Amo 2:12; Yer 38:4; Ay 21:18; Yer 21:7; 34:20; Isa 30:10
[h]**11:22** Isa 9:17; Yer 18:21
[i]**11:23** Lk 19:44; Yer 6:9; 23:12
[j]**12:1** Ay 8:3; 12:6; Dan 9:14; Ay 21:7, 13; Ezr 9:15; Ay 5:8; Eze 18:25; Yer 5:27-28
[k]**12:2** Isa 29:13; Eze 22:27; Yer 11:17; Mk 7:6; Ay 5:3; Yer 3:10; Mt 15:8; Tit 1:16

3 [a]Hata hivyo unanijua mimi, Ee BWANA;
unaniona na kuyachunguza mawazo yangu kukuhusu wewe.
Wakokote kama kondoo wanaokwenda kuchinjwa!
Watenge kwa ajili ya siku ya kuchinjwa!
4 [b]Je, nchi itakaa katika hali ya kuomboleza mpaka lini,
na majani katika kila shamba kunyauka?
Kwa sababu wale waishio ndani yake ni waovu,
wanyama na ndege wameangamia.
Zaidi ya hayo, watu wanasema,
"BWANA hataona yatakayotupata sisi."

*Jibu La Mungu*

5 [c]"Ikiwa umeshindana mbio na watu kwa mguu na wakakushinda,
unawezaje kushindana na farasi?
Ikiwa unajikwaa kwenye nchi ambayo ni salama,
utawezaje kwenye vichaka kando ya Yordani?
6 [d]Ndugu zako, watu wa jamaa yako mwenyewe:
hata wao wamekusaliti;
wameinua kilio kikubwa dhidi yako.
Usiwaamini, ingawa wanazungumza mema juu yako.

7 "Nitaiacha nyumba yangu,
nitupe urithi wangu;
nitamtia yeye nimpendaye mikononi mwa adui zake.
8 [e]Urithi wangu umekuwa kwangu kama simba wa msituni.
Huningurumia mimi,
kwa hiyo ninamchukia.
9 [f]Je, urithi wangu haukuwa kama ndege wa mawindo wa madoadoa
ambaye ndege wengine wawindao humzunguka na kumshambulia?
Nenda ukawakusanye pamoja wanyama wote wa mwituni;
walete ili wale.
10 [g]Wachungaji wengi wataliharibu shamba langu la mizabibu
na kulikanyaga shamba langu;
watalifanya shamba langu zuri kuwa jangwa la ukiwa.
11 [h]Litafanywa kuwa jangwa,
lililokauka na kuachwa ukiwa mbele zangu;
nchi yote itafanywa jangwa
kwa sababu hakuna hata mmoja anayejali.
12 [i]Juu ya miinuko yote ilivyo kama jangwani
mharabu atajaa,
kwa maana upanga wa BWANA utawala,
kuanzia ncha moja ya nchi hadi nyingine;
hakuna hata mmoja atakayekuwa salama.
13 [j]Watapanda ngano lakini watavuna miiba;
watajitaabisha lakini hawatafaidi chochote.
Kwa hiyo beba aibu ya mavuno yako
kwa sababu ya hasira kali ya BWANA Mungu."

14 [k]Hili ndilo asemalo BWANA: "Kwa

[a]**12:3** Yer 17:18; Za 7:9; 11:5; Yer 20:11; 16:18
[b]**12:4** Yer 4:25-28; Yoe 1:10-12; Kum 28:15-18; Za 107:34; Yer 4:26; 9:10
[c]**12:5** Yer 49:19; 50:44
[d]**12:6** Mit 26:24-25; Yer 9:4; Za 12:2
[e]**12:8** Amo 6:8; 2Nya 36:16; Za 17:12; Hos 9:15
[f]**12:9** Kum 28:26; Isa 56:9; Yer 15:3; Eze 23:25; 39:17-20
[g]**12:10** Yer 25:34; Eze 33:2; Isa 5:1-7; Yer 9:10; 25:11
[h]**12:11** Isa 42:25; Yer 23:10; Isa 5:6; 24:4; Yer 9:12; 14:4
[i]**12:12** Kum 32:41; Eze 33:2; Yer 3:2; Eze 21:3-4; Isa 31:8; Yer 46:10; Eze 14:17
[j]**12:13** Mik 6:15; Kut 15:7; Yer 4:26; Law 26:16-20; Kum 28:38
[k]**12:14** Zek 2:7-9; Sef 2:8-10; Yer 32:37; 2Nya 7:20; Za 9:6; Kum 29:28

habari ya majirani zangu wote wabaya
wanaonyang'anya urithi ambao ninawapa
watu wangu Israeli, nitawang'oa kutoka
nchi zao, nami nitaing'oa nyumba ya
Yuda kutoka katikati yao. 15 [a]Lakini baada
ya kuwang'oa, nitawahurumia tena na
kumrudisha kila mmoja wao kwenye
urithi wake mwenyewe na kwenye nchi
yake mwenyewe. 16 [b]Ikiwa watajifunza
vyema njia za watu wangu na kuapa
kwa Jina langu, wakisema, 'Hakika kama
BWANA aishivyo,' hata kama wakati fulani
walifundisha watu wangu kuapa kwa Baali,
ndipo watakapofanywa imara katikati ya
watu wangu. 17 [c]Lakini kama taifa lolote
halitasikiliza na kutii, nitaling'oa kabisa
na kuliangamiza," asema BWANA.

### *Mkanda Wa Kitani*

13 Hili ndilo BWANA aliloniambia: "Nenda
ununue mkanda wa kitani, ujivike
kiunoni mwako, lakini usiuache uguse
maji." 2 Kwa hiyo nikanunua mkanda, kama
BWANA alivyoniagiza, nikajivika kiunoni.
3 [d]Ndipo neno la BWANA likanijia kwa
mara ya pili: 4 [e]"Chukua mkanda ulionunua
ambao umeuvaa kiunoni mwako, uende
sasa Frati uufiche ndani ya ufa mdogo
kwenye mwamba." 5 [f]Ndipo nikaenda na
kuuficha ule mkanda huko Frati, kama
BWANA alivyoniamuru.
6 Baada ya siku nyingi BWANA
akaniambia, "Nenda sasa Frati ukauchukue
ule mkanda niliokuambia uufiche huko."
7 [g]Hivyo nikaenda Frati na kuuchimbua ule
mkanda kutoka pale nilipokuwa nimeuficha,
lakini sasa ulikuwa umeharibika na haufai
tena kabisa.
8 Ndipo neno la BWANA likanijia: 9 [h]"Hili
ndilo BWANA asemalo: 'Vivyo hivyo ndivyo
nitakavyokiharibu kiburi cha Yuda na
kiburi kikuu cha Yerusalemu. 10 [i]Watu hawa
waovu, wanaokataa kusikiliza maneno
yangu, wafuatao ukaidi wa mioyo yao na
kufuata miungu mingine kuitumikia na
kuiabudu, watakuwa kama mkanda huu
ambao haufai kabisa! 11 [j]Kwa maana kama
vile mkanda ufungwavyo kiunoni mwa
mtu, ndivyo nilivyojifunga nyumba yote
ya Israeli na nyumba yote ya Yuda,' asema
BWANA, 'ili wawe watu wangu kwa ajili
ya utukufu wangu, sifa na heshima yangu.
Lakini hawajasikiliza.'

### *Viriba Vya Mvinyo*

12 "Waambie: 'Hili ndilo BWANA, Mungu
wa Israeli, asemalo: kila kiriba inapasa
kijazwe mvinyo.' Kama wao wakikuambia,
'Kwani hatujui kwamba kila kiriba inapasa
kijazwe mvinyo?' 13 [k]Kisha uwaambie, 'Hili
ndilo asemalo BWANA: nitawajaza ulevi
wote waishio katika nchi hii, pamoja na
wafalme waketio juu ya kiti cha enzi cha
Daudi, makuhani, manabii na wale wote
waishio Yerusalemu. 14 [l]Nitawagonganisha
kila mmoja na mwenzake, baba na wana
wao, asema BWANA. Sitawarehemu wala
kuwahurumia ili niache kuwaangamiza.' "

### *Tishio La Kutekwa*

15 Sikieni na mzingatie,
msiwe na kiburi,
kwa kuwa BWANA amenena.
16 [m]Mpeni utukufu BWANA Mungu
wenu,
kabla hajaleta giza,
kabla miguu yenu haijajikwaa
juu ya vilima vitakavyotiwa giza.

[a]**12:15** Kum 30:3; Amo 9:14-15; Eze 28:25; Za 6:2
[b]**12:16** Yer 4:2; Yos 23:7; Efe 2:20; Isa 26:18; 49:6; Yer 18:8; 3:17
[c]**12:17** Mwa 27:29; Isa 60:12; Za 2:8-9
[d]**13:3** Yer 33:1
[e]**13:4** Mwa 2:14
[f]**13:5** Kut 40:16
[g]**13:7** Isa 64:6; Yer 24:8; Mao 3:45
[h]**13:9** Law 26:19; Mt 23:12; Lk 1:51
[i]**13:10** Mhu 9:3; Yer 16:12; Kum 8:19; 9:14; 22:21; 3:17; Amu 10:13; Eze 15:3
[j]**13:11** Kut 19:5-6; Isa 63:12; 43:21; 65:12; Yer 33:9; 7:26; 32:20
[k]**13:13** Za 60:3; Isa 29:9; Eze 23:32-34; Za 75:8; Yer 25:18; 51:57
[l]**13:14** Isa 9:17; Yer 16:5; Isa 9:19-21; Mao 2:21; Eze 7:4; Zek 11:6
[m]**13:16** Yos 7:19; Law 26:37; 1Sam 2:9; Isa 59:9; Yer 23:12; Za 82:5

Mlitarajia nuru,
lakini ataifanya kuwa giza nene
na kuibadili kuwa huzuni kubwa.
17 [a]Lakini kama hamtasikiliza,
nitalia sirini
kwa ajili ya kiburi chenu;
macho yangu yatalia kwa uchungu,
yakitiririka machozi,
kwa sababu kundi la kondoo la
Bwana
litachukuliwa mateka.

18 [b]Mwambie mfalme na mamaye,
"Shukeni kutoka kwenye viti
vyenu vya enzi,
kwa kuwa taji zenu za utukufu
zitaanguka kutoka vichwani
mwenu."
19 [c]Miji iliyoko Negebu itafungwa,
wala hapatakuwa na mtu wa
kuifungua.
Watu wa Yuda wote watapelekwa
uhamishoni,
wakichukuliwa kabisa waende
mbali.

20 [d]Inua macho yako uone
wale wanaokuja kutoka kaskazini.
Liko wapi lile kundi ulilokabidhiwa,
kondoo wale uliojivunia?
21 [e]Utasema nini Bwana
atakapowaweka juu yako
wale ulioungana nao kama
marafiki wako maalum?
Je, hutapatwa na utungu kama
mwanamke
aliye katika utungu wa kuzaa?
22 [f]Nawe kama ukijiuliza,
"Kwa nini haya yamenitokea?"
Ni kwa sababu ya dhambi zako
nyingi
ndipo marinda yako yameraruliwa
na mwili wako umetendewa
vibaya.
23 Je, Mkushi aweza kubadili ngozi
yake
au chui kubadili madoadoa yake?
Vivyo hivyo nawe huwezi kufanya
mema
wewe uliyezoea kutenda mabaya.

24 [g]"Nitawatawanya kama makapi
yapeperushwayo na upepo wa
jangwani.
25 [h]Hii ndiyo kura yako,
fungu nililokuamuria,"
asema Bwana,
"kwa sababu umenisahau mimi
na kuamini miungu ya uongo.
26 [i]Nitayafunua marinda yako mpaka
juu ya uso wako
ili aibu yako ionekane:
27 [j]uzinzi wako na kulia kwako kama
farasi kulikojaa tamaa,
ukahaba wako usio na aibu!
Nimeyaona matendo yako ya
machukizo
juu ya vilima na mashambani.
Ole wako, ee Yerusalemu!
Utaendelea kuwa najisi mpaka
lini?"

*Ukame, Njaa Na Upanga*

14 Hili ndilo neno la Bwana kwa Yeremia kuhusu ukame:

2 [k]"Yuda anaomboleza,
miji yake inayodhoofika;
wanaomboleza kwa ajili ya nchi,
nacho kilio kinapanda kutoka
Yerusalemu.

[a]**13:17** Yer 14:18; Mal 2:2; Za 80:1; Yer 29:1
[b]**13:18** Yer 21:11; Mao 5:16; 2Fal 24:18; 2:19; Eze 16:12
[c]**13:19** Yer 52:30; Law 26:31; Yer 20:4
[d]**13:20** Yer 6:22; 23:2; Hab 1:6
[e]**13:21** Za 41:9; Oba 1:7; Yer 4:30; 20:10; 38:22; 4:31
[f]**13:22** Yer 9:2-6; 16:10-12; Nah 3:5-6; 1Fal 9:9; Isa 20:4; Eze 16:37; 23:26
[g]**13:24** Ay 27:21; 1:19; Law 26:33
[h]**13:25** Ay 20:29; Mt 24:51; Mik 3:11; Isa 17:10; Za 106:19-21
[i]**13:26** Mao 1:6-8; Hos 2:10; Eze 16:37; Nah 3:5
[j]**13:27** Yer 2:20; Eze 23:29; 6:13; Hos 8:5; Isa 57:7
[k]**14:2** Isa 3:26; Yer 8:21; Mit 21:13

3 [a]Wakuu wanawatuma watumishi wao
maji;
wanakwenda visimani
lakini humo hakuna maji.
Wanarudi na vyombo bila maji;
wakiwa na hofu na kukata tamaa,
wanafunika vichwa vyao.
4 [b]Ardhi imepasuka nyufa
kwa sababu hakuna mvua katika
nchi;
wakulima wana hofu
na wanafunika vichwa vyao.
5 [c]Hata kulungu mashambani
anamwacha mtoto wake
aliyezaliwa wakati huo huo
kwa sababu hakuna majani.
6 [d]Punda-mwitu wanasimama juu ya
miinuko iliyo kame
na kutweta kama mbweha;
macho yao yanakosa nguvu za kuona
kwa ajili ya kukosa malisho."

7 [e]Ingawa dhambi zetu zinashuhudia
juu yetu,
Ee BWANA, tenda jambo kwa ajili
ya jina lako.
Kwa kuwa kukengeuka kwetu ni
kukubwa,
nasi tumetenda dhambi dhidi
yako.
8 [f]Ee Tumaini la Israeli,
Mwokozi wake wakati wa taabu,
kwa nini unakuwa kama mgeni
katika nchi,
kama msafiri anayekaa kwa usiku
mmoja tu?
9 [g]Mbona unakuwa kama mtu
aliyeshtukizwa,
kama shujaa asiye na uwezo wa
kuokoa?
Wewe uko katikati yetu, Ee BWANA,
nasi tunaitwa kwa jina lako;
usituache!

10 [h]Hili ndilo BWANA asemalo kuhusu
watu hawa:

"Wanapenda sana kutangatanga,
hawaizuii miguu yao.
Hivyo BWANA hawakubali;
sasa ataukumbuka uovu wao
na kuwaadhibu kwa ajili ya
dhambi zao."

11 [i]Kisha BWANA akaniambia, "Usiombe
kwa ajili ya mafanikio ya watu hawa.
12 [j]Ingawa wanafunga, sitasikiliza kilio
chao; hata wakitoa dhabihu za kuteketezwa
na dhabihu za nafaka, sitazikubali. Badala
yake, nitawaangamiza kwa upanga, njaa
na tauni."
13 Lakini nikasema, "Aa, BWANA
Mwenyezi, manabii wanaendelea
kuwaambia, 'Hamtaona upanga wala
kukabiliwa na njaa. Naam, nitawapa amani
ya kudumu mahali hapa.' "
14 [k]Ndipo BWANA akaniambia, "Manabii
wanatabiri uongo kwa jina langu.
Sikuwatuma, wala sikuwaweka, wala
sikusema nao. Wanawatabiria maono ya
uongo, maaguzi, maono ya sanamu zisizofaa
kitu, na madanganyo ya mawazo yao
wenyewe.
15 [l]Kwa hiyo, hili ndilo BWANA
asemalo kuhusu manabii wanaotabiri
kwa jina langu: Mimi sikuwatuma, lakini

[a]**14:3** Kum 28:48; 2Fal 18:31; 2Sam 15:30; Es 6:12; Ay 6:19-20
[b]**14:4** Amo 4:8; Zek 14:17; Yer 3:3; 12:11
[c]**14:5** Isa 15:6
[d]**14:6** Ay 39:5-6; Yer 2:24; Za 104:11; Mwa 47:4
[e]**14:7** Isa 3:9; Hos 5:5; Yer 2:19; 8:14; Za 25:11; 79:9; 1Sam 12:22
[f]**14:8** Za 9:18; Mdo 28:20; Yer 17:13; 50:7; Za 18:46; Isa 25:9
[g]**14:9** Isa 50:2; Mwa 17:7; Yer 8:19; 15:16; Kut 29:45; Isa 63:19; Za 27:9
[h]**14:10** Yer 2:25; Za 119:101; Yer 6:20; Hes 8:13; Ebr 8:12; Amo 5:22; Hos 7:2; 9:9; Yer 44:21
[i]**14:11** Kut 32:10; 1Sam 2:25
[j]**14:12** Kum 1:45; 1Sam 8:18; Yer 7:21; Law 1:1-17; Yer 11:11; Amo 5:22; Isa 51:19; Yer 9:16
[k]**14:14** Yer 23:25; 2The 2:9-11; Eze 13:2-6; Yer 23:16; Mao 2:9; Eze 12:24; Yer 27:14
[l]**14:15** Yer 20:6; Eze 14:9; Yer 16:4; Mao 1:19; Yer 23:15; 5:12-13

wanasema, 'Hakuna upanga wala njaa itakayoigusa nchi hii.' Manabii hao hao watakufa kwa upanga na njaa.
16 [a]Nao watu hao wanaowatabiria watatupwa nje katika barabara za Yerusalemu kwa sababu ya njaa na upanga. Hapatakuwepo yeyote wa kuwazika wao au wake zao, wana wao au binti zao. Nitawamwagia maafa wanayostahili.
17 [b]"Nena nao neno hili:

" 'Macho yangu na yatiririkwe na machozi
usiku na mchana bila kukoma;
kwa kuwa binti yangu aliye bikira, yaani watu wangu,
amepata jeraha baya,
pigo la kuangamiza.
18 [c]Kama nikienda mashambani,
ninaona wale waliouawa kwa upanga;
kama nikienda mjini,
ninaona maangamizi ya njaa.
Nabii na kuhani kwa pamoja
wamekwenda katika nchi wasiyoijua.' "

19 [d]Je, umemkataa Yuda kabisa?
Umemchukia Sayuni kabisa?
Kwa nini umetuumiza
hata hatuwezi kuponyeka?
Tulitarajia amani,
lakini hakuna jema lililotujia;
tulitarajia wakati wa kupona
lakini kuna hofu kuu tu.
20 [e]Ee Bwana, tunatambua uovu wetu
na kosa la baba zetu;
kweli tumetenda dhambi dhidi yako.
21 [f]Kwa ajili ya jina lako usituchukie kabisa;
usikidharau kiti chako cha enzi kilichotukuka.
Kumbuka agano lako nasi
na usilivunje.
22 [g]Je, kuna sanamu yoyote isiyofaa kitu ya mataifa
iwezayo kuleta mvua?
Je, anga peke yake zaweza kutoa mvua?
La hasha, ni wewe peke yako,
Ee Bwana, Mungu wetu.
Kwa hiyo tumaini letu liko kwako,
kwa kuwa wewe ndiwe ufanyaye haya yote.

*Adhabu Isiyoepukika*

15 [h]Kisha Bwana akaniambia: "Hata kama Mose na Samweli wangesimama mbele zangu, moyo wangu usingewaelekea watu hawa. Waondoe mbele za macho yangu! Waache waende!
2 [i]Nao kama wakikuuliza, 'Twende wapi?' Waambie, 'Hili ndilo Bwana asemalo:

" 'Wale waliowekwa kwa ajili ya kufa, wakafe;
waliowekwa kwa ajili ya upanga, kwa upanga;
waliowekwa kwa ajili ya njaa, kwa njaa:
waliowekwa kwa ajili ya kutekwa, watekwe.' "

3 [j]Bwana asema, "Nitatuma aina nne za waharabu dhidi yao: nazo ni upanga ili kuua na mbwa ili wakokote mbali, ndege wa angani na wanyama wa nchi ili kula na kuangamiza.
4 [k]Nitawafanya

[a]**14:16** Yer 17:10; Mit 1:31; Yer 7:33; Za 79:3; Mt 15:14
[b]**14:17** Za 119:136; Yer 8:21; Mao 1:16; 2Fal 19:21; Yer 23:12
[c]**14:18** Eze 7:14-15; 2Nya 36:10; Yer 13:17
[d]**14:19** Yer 7:29; 30:12-13; 8:15; Isa 1:6
[e]**14:20** Amu 10:10; Dan 9:7-8; Yer 3:13; Law 26:40; 1Fal 8:47; Ezr 9:6
[f]**14:21** Yer 17:12; Yos 7:9; Isa 62:7; Yer 3:17; Kut 2:24
[g]**14:22** 1Fal 8:36; Isa 30:23; Za 135:7; Isa 41:24; 44:10; Yer 10:15
[h]**15:1** Kut 32:11; Hes 14:13-20; 1Sam 7:9; Eze 14:14, 20; 2Fal 17:20; Yer 16:13; 7:16
[i]**15:2** Yer 42:22; 44:13; Zek 11:9; Mao 4:9; Eze 12:11; Ufu 13:10; Yer 14:12
[j]**15:3** Law 26:16; Hes 33:4; Kum 28:26; Eze 33:27; 14:21; 2Fal 9:36; 1Fal 21:19
[k]**15:4** Eze 23:46; Yer 29:18; 34:17; Ay 17:6; 2Fal 21:2, 11; 23:26-27; Yer 24:9

wawe machukizo kwa falme zote za dunia kwa sababu ya kile alichofanya Manase mwana wa Hezekia mfalme wa Yuda huko Yerusalemu.

5 [a]"Ni nani atakayekuhurumia, ee
Yerusalemu?
Ni nani atakayeomboleza kwa ajili
yako?
Ni nani atakayesimama ili kuuliza
kuhusu hali yako?
6 [b]Umenikataa mimi," asema BWANA.
"Unazidi kukengeuka.
Hivyo nitanyoosha mkono wangu
juu yako na kukuangamiza,
siwezi kuendelea kukuonea
huruma.
7 [c]Nitawapepeta kwa uma wa
kupepetea
kwenye malango ya miji katika
nchi.
Nitaleta msiba na maangamizi juu ya
watu wangu,
kwa maana hawajabadili njia zao.
8 [d]Nitawafanya wajane wao kuwa
wengi
kuliko mchanga wa bahari.
Wakati wa adhuhuri nitamleta
mharabu
dhidi ya mama wa vijana wao
waume;
kwa ghafula nitaleta juu yao
maumivu makuu na hofu kuu.
9 [e]Mama mwenye watoto saba
atazimia
na kupumua pumzi yake ya
mwisho.
Jua lake litatua kungali bado
mchana,
atatahayarika na kufedheheka.
Wale wote waliobaki nitawaua kwa
upanga
mbele ya adui zao,"
asema BWANA.

10 [f]Ole wangu, mama yangu, kwamba
ulinizaa,
mtu ambaye ulimwengu wote
unashindana na kugombana naye!
Sikukopa wala sikukopesha,
lakini kila mmoja ananilaani.

11 [g]BWANA akasema,

"Hakika nitakuokoa kwa kusudi
jema,
hakika nitawafanya adui zako
wakuombe msaada
nyakati za maafa na nyakati za
dhiki.

12 [h]"Je, mtu aweza kuvunja chuma,
chuma kitokacho kaskazini, au
shaba?
13 [i]Utajiri wako na hazina zako
nitavitoa kuwa nyara,
bila gharama,
kwa sababu ya dhambi zako zote
katika nchi yako yote.
14 [j]Nitakufanya uwe mtumwa wa adui
zako
katika nchi usiyoijua,
kwa kuwa katika hasira yangu moto
umewashwa
utakaowaka juu yako daima."

15 [k]Wewe unafahamu, Ee BWANA,
unikumbuke na unitunze mimi.
Lipiza kisasi juu ya watesi wangu.
Kwa uvumilivu wako usiniondolee
mbali;
kumbuka jinsi ninavyoshutumiwa.

---

[a]**15:5** Isa 27:11; Nah 3:7; Isa 51:19; Yer 13:14; 16:13; 21:7
[b]**15:6** Kum 32:15; Yer 6:19; Isa 31:3; Hos 13:14; Yer 7:20; Amo 7:8
[c]**15:7** Isa 9:13; Yer 18:21; Isa 41:16; 3:26; 2Nya 28:22
[d]**15:8** Isa 47:9; Yer 6:4; Ay 18:11
[e]**15:9** 1Sam 2:5; Yer 21:7; 25:31; 7:19; Amo 8:9; 2Fal 25:7; Yer 19:7
[f]**15:10** Ay 10:18-19; Law 25:36; Neh 5:1-12; Ay 3:1; Yer 6:10; 1:19
[g]**15:11** Yer 40:4; 37:3; 42:1-3; 21:1-2
[h]**15:12** Mao 1:14; Hos 10:11; Kum 28:48; Yer 28:14
[i]**15:13** Yer 17:3; Za 44:12; Eze 38:12-13; 2Fal 24:13; 25:15
[j]**15:14** Kum 28:36; Yer 16:13; Kum 32:22; Za 21:9; Yer 5:19
[k]**15:15** Yn 21:15-17; Yer 12:3; Za 69:7-9; 119:84; 44:22; Kut 34:6

16 [a]Maneno yako yalipokuja, niliyala;
yakawa shangwe yangu
na furaha ya moyo wangu,
kwa kuwa nimeitwa kwa jina lako,
Ee BWANA Mungu Mwenye Nguvu
Zote.
17 [b]Kamwe sikuketi katika kundi la
wafanyao sherehe,
wala kamwe sikujifurahisha
pamoja nao;
niliketi peke yangu kwa sababu
mkono wako ulikuwa juu
yangu,
na wewe ulikuwa umenijaza
hasira.
18 [c]Kwa nini maumivu yangu
hayakomi,
na jeraha langu ni la kuhuzunisha,
wala haliponyeki?
Je, utakuwa kwangu kama kijito cha
udanganyifu,
kama chemchemi iliyokauka?

19 [d]Kwa hiyo hili ndilo asemalo BWANA:

“Kama ukitubu, nitakurejeza
ili uweze kunitumikia;
kama ukinena maneno yenye maana,
wala si ya upuzi,
utakuwa mnenaji wangu.
Watu hawa ndio watakaokugeukia,
wala si wewe utakayewageukia
wao.
20 [e]Nitakufanya wewe uwe ukuta kwa
watu hawa,
ngome ya ukuta wa shaba;
watapigana nawe
lakini hawatakushinda,
kwa maana mimi niko pamoja nawe
kukuponya na kukuokoa,”
asema BWANA.
21 [f]“Nitakuokoa kutoka mikono ya
waovu,
na kukukomboa kutoka makucha
ya watu wakatili.”

*Siku Ya Maafa*

16 Kisha neno la BWANA likanijia:
2 [g]“Kamwe usioe na kuwa na wana
wala binti mahali hapa.” 3 [h]Kwa maana
hili ndilo asemalo BWANA kuhusu wana
na binti wazaliwao katika nchi hii, na
kuhusu wale wanawake ambao ni mama
zao, na wale wanaume ambao ni baba zao:
4 [i]“Watakufa kwa magonjwa ya kufisha.
Hawataombolezewa wala kuzikwa, lakini
watakuwa kama mavi yaliyosambaa juu ya
ardhi. Watakufa kwa upanga na kwa njaa,
nazo maiti zao zitakuwa chakula cha ndege
wa angani, na cha wanyama wa nchi.”
5 Kwa kuwa hili ndilo asemalo BWANA:
“Usiingie katika nyumba ambayo
kuna chakula cha matanga, usiende
kuwaombolezea wala kuwahurumia, kwa
sababu nimeziondoa baraka zangu, upendo
wangu na huruma zangu kutoka kwa
watu hawa,” asema BWANA. 6 [j]“Wakubwa
na wadogo watakufa katika nchi hii.
Hawatazikwa wala kuombolezewa, na
hakuna atakayejikatakata au kunyoa
nywele za kichwa chake kwa ajili yao.
7 [k]Hakuna yeyote atakayewapa chakula
ili kuwafariji wale waombolezao kwa ajili
ya wale waliokufa, hata akiwa amefiwa
na baba au mama, wala hakuna yeyote
atakayewapa kinywaji ili kuwafariji.
8 [l]“Usiingie katika nyumba ambayo kuna
karamu, na kuketi humo ili kula na kunywa.
9 [m]Kwa kuwa hili ndilo asemalo BWANA

[a]**15:16** Ay 23:12; 15:11; Eze 2:8; Ufu 10:10; Za 119:72, 103; Yer 14:9; Isa 43:7
[b]**15:17** Rut 3:3; Za 26:4-5; Yer 16:8; 2Fal 3:15
[c]**15:18** Mik 1:9; Ay 6:4; Za 9:10
[d]**15:19** Zek 3:7; Eze 22:26; Kut 4:16
[e]**15:20** Yer 42:11; Eze 3:8; Isa 50:7; Za 129:2; Yer 20:11
[f]**15:21** Yer 50:34; Mwa 48:16; Isa 49:25; Yer 1:8; Za 97:10
[g]**16:2** Mwa 19:14; Mt 19:12; 1Kor 7:26-27
[h]**16:3** Yer 6:21
[i]**16:4** Yer 25:33; 9:22; Za 83:10; Kum 28:26; Za 79:1-3; Yer 14:15; 19:7
[j]**16:6** Yer 9:21; Eze 9:5-6; Law 19:28; 21:5; Isa 22:12; 1:20
[k]**16:7** Mit 3:6; Eze 24:17; Hos 9:4; 2Sam 3:35; Yer 22:10; Mao 1:9, 16
[l]**16:8** Kut 32:6; Mhu 7:2-4; Yer 15:17
[m]**16:9** Isa 51:3; Amo 6:4-7; Yer 7:34; Isa 22:12-14; Ufu 18:23; Eze 26:13

Mwenye Nguvu Zote, aliye Mungu wa
Israeli: ‘Mbele ya macho yako na katika siku
zako, nitakomesha sauti zote za shangwe
na za furaha, na pia sauti za bibi arusi na
bwana arusi mahali hapa.’
10 [a]“Utakapowaambia watu hawa
mambo haya yote na wakakuuliza, ‘Kwa
nini BWANA ameamuru maafa makubwa
kama haya dhidi yetu? Tumefanya kosa
gani? Tumetenda dhambi gani dhidi ya
BWANA, Mungu wetu?’ 11 [b]Basi waambie,
‘Ni kwa sababu baba zenu waliniacha
mimi, wakafuata miungu mingine ili
kuitumikia na kuiabudu. Waliniacha
mimi na hawakuishika sheria yangu,’
asema BWANA. 12 [c]“Lakini ninyi mmetenda
uovu zaidi kuliko baba zenu. Tazama jinsi
ambavyo kila mmoja wenu anafuata ukaidi
wa moyo wake mbaya, badala ya kunitii
mimi. 13 [d]Kwa hiyo nitawaondoa katika
nchi hii na kuwatupa katika nchi ambayo
ninyi wala baba zenu hamkuijua, nako
huko mtaitumikia miungu mingine usiku
na mchana, kwa maana sitawapa fadhili
zangu huko.’
14 [e]“Hata hivyo, siku zinakuja,” asema
BWANA, “wakati ambapo watu hawatasema
tena, ‘Hakika kama BWANA aishivyo,
aliyewapandisha Waisraeli kutoka Misri,’
15 [f]bali watasema, ‘Hakika kama BWANA
aishivyo, aliyewatoa wana wa Israeli kutoka
nchi ya kaskazini na nchi zote alizokuwa
amewafukuzia.’ Maana nitawarudisha
katika nchi niliyowapa baba zao.
16 [g]“Lakini sasa nitawaagiza wavuvi
wengi,” asema BWANA, “nao watawavua.
Baada ya hilo, nitawaagizia wawindaji
wengi, nao watawawinda kwenye kila
mlima na kilima, na katika nyufa za
miamba. 17 [h]Macho yangu yanaziona njia
zao zote, hazikufichika kwangu, wala
dhambi yao haikusitirika. 18 [i]Nitawalipiza
maradufu kwa ajili ya uovu wao na dhambi
yao, kwa sababu wameinajisi nchi yangu
kwa maumbo yasiyo na uhai ya vinyago
vyao vibaya, na kuujaza urithi wangu na
sanamu za kuchukiza.”

19 [j]Ee BWANA, nguvu zangu na ngome
yangu,
kimbilio langu wakati wa taabu,
kwako mataifa yatakujia
kutoka miisho ya dunia na
kusema,
“Baba zetu hawakuwa na chochote
zaidi ya miungu ya uongo,
sanamu zisizofaa kitu
ambazo hazikuwafaidia lolote.
20 [k]Je, watu hujitengenezea miungu yao
wenyewe?
Naam, lakini hao si miungu!”

21 [l]“Kwa hiyo nitawafundisha:
wakati huu nitawafundisha
nguvu zangu na uwezo wangu.
Ndipo watakapojua
kuwa Jina langu ndimi BWANA.

### *Dhambi Ya Yuda Na Adhabu Yake*

17 [m]“Dhambi ya Yuda imechorwa
kwa kalamu ya chuma,
imeandikwa kwa ncha ya almasi,
kwenye vibao vya mioyo yao
na kwenye pembe za madhabahu
zao.

[a]**16:10** Kum 29:24; Yer 5:19
[b]**16:11** Amu 2:12-13; Za 106:35-43; 1Fal 9:9; Neh 9:26-29; Ay 31:27; Kum 29:25-26
[c]**16:12** Kut 32:8; Amo 2:4; Mhu 9:3; Yer 13:10; 2Tim 3:13; Yer 7:26; Eze 20:30
[d]**16:13** Kum 4:26-28; Yer 15:4-5; 2Nya 20:7; Yer 5:19; Kum 28:36
[e]**16:14** Kum 15:15; Yer 23:7-8; 29:10; 31:27, 38; 30:3
[f]**16:15** Isa 11:11-12; Za 53:6; Yer 3:18; 23:8; 30:3; Eze 38:14; Yoe 3:1; Kum 30:3
[g]**16:16** Amo 4:2; Hab 1:14-15; Amo 9:3; Mik 7:2; 1Sam 26:20
[h]**16:17** Mhu 12:14; Mk 4:22; Mit 5:21; Sef 1:12; Yer 32:19; Mwa 3:8; Ebr 4:13
[i]**16:18** Hes 35:34; Isa 40:2; Eze 43:7; Ufu 18:6; Isa 65:6; Yer 12:3; Za 101:3
[j]**16:19** Yer 3:17; Za 4:2; Isa 2:2; Za 18:2; 2Sam 22:3; Yer 14:22; Isa 40:19; 1Sam 12:21
[k]**16:20** Isa 37:19; Rum 1:23; Gal 4:8; Za 115:4-7; Yer 2:11
[l]**16:21** Kut 3:15
[m]**17:1** Ay 19:24; 2Kor 3:3; Mit 3:3; Kum 6:6; Kut 27:2

2 [a]Hata watoto wao wanakumbuka
madhabahu zao
na nguzo za Ashera,[b]
kandokando ya miti iliyotanda
na juu ya vilima virefu.
3 [c]Mlima wangu katika nchi pamoja na
utajiri
na hazina zako zote nitazitoa ziwe
nyara,
pamoja na mahali pako pa juu pa
kuabudia miungu
kwa sababu ya dhambi katika nchi
yako yote.
4 [d]Kwa kosa lako mwenyewe
utaupoteza
urithi niliokupa.
Nitakufanya mtumwa wa adui zako
katika nchi usiyoijua,
kwa kuwa umeiwasha hasira yangu,
nayo itawaka milele."

5 [e]Hili ndilo asemalo BWANA:

"Amelaaniwa yeye amtegemeaye
mwanadamu,
ategemeaye mwenye mwili
kwa ajili ya nguvu zake,
ambaye moyo wake
umemwacha BWANA.
6 [f]Atakuwa kama kichaka cha
jangwani;
hataona mafanikio yatakapokuja.
Ataishi katika sehemu zisizo na maji,
katika nchi ya chumvi ambapo
hakuna yeyote aishiye humo.

7 [g]"Lakini amebarikiwa mtu ambaye
tumaini lake ni katika
BWANA,
ambaye matumaini yake ni katika
BWANA.
8 [h]Atakuwa kama mti uliopandwa
kando ya maji
uenezao mizizi yake karibu na
kijito cha maji.
Hauogopi wakati wa joto ujapo;
majani yake ni mabichi daima.
Hauna hofu katika mwaka wa ukame
na hautaacha kuzaa matunda."

9 [i]Moyo ni mdanganyifu kuliko vitu
vyote,
ni mwovu kupita kiasi.
Ni nani awezaye kuujua?

10 [j]"Mimi BWANA huchunguza moyo
na kuzijaribu nia,
ili kumlipa mtu kwa kadiri ya
mwenendo wake,
kwa kadiri ya matendo yake
yanavyostahili."

11 [k]Kama kware aanguaye mayai
asiyoyataga,
ndivyo alivyo mtu apataye mali
kwa njia zisizo za haki.
Maisha yake yafikapo katikati, siku
zitamwacha,
na mwishoni atabainika kuwa
mpumbavu.

12 [l]Kiti cha enzi kilichotukuzwa,
kilichoinuliwa tangu mwanzo,
ndiyo sehemu yetu ya mahali
patakatifu.
13 [m]Ee BWANA, uliye tumaini la Israeli,
wote wakuachao wataaibika.

---

[a]**17:2** 2Nya 24:18; 2Fal 16:4; Yer 2:20
[b]2 Ashera ni mungu mke aliyekuwa anaabudiwa na Wakanaani.
[c]**17:3** 2Fal 24:13; Yer 15:13; Mik 3:12; Yer 26:18
[d]**17:4** Mao 5:2; Yer 12:7; 16:13; 22:28; 7:20; 15:14; Kum 28:48
[e]**17:5** Za 108:12; Isa 30:1-3; 2:22; 2Kor 1:9
[f]**17:6** Kum 29:23; Za 107:34; Ay 20:17; 20:17; 30:3; 39:6; Yer 48:9
[g]**17:7** Mit 16:20; Za 146:5; 34:8; 40:4; Yer 39:18
[h]**17:8** Yer 14:1-6; Eze 47:12; Ay 14:9; Za 92:12-14; Eze 19:10
[i]**17:9** Mhu 9:3; Mt 13:15; Mk 7:21-22
[j]**17:10** Yos 22:22; Mit 17:3; Ufu 2:23; Eze 11:5; Rum 8:27; Za 62:12; Yer 32:19; Rum 2:6
[k]**17:11** Lk 12:20
[l]**17:12** Yer 3:17
[m]**17:13** Za 71:5; 73:27; Yer 14:8; 2:17; Za 69:28; Eze 13:9; Isa 12:3; Yn 4:10

Wale wanaogeukia mbali nawe
wataandikwa mavumbini
kwa sababu wamemwacha
BWANA,
chemchemi ya maji yaliyo hai.

14 [a]Uniponye, Ee BWANA, nami
nitaponyeka;
uniokoe nami nitaokoka,
kwa maana wewe ndiwe
ninayekusifu.
15 [b]Wao huendelea kuniambia,
"Liko wapi neno la BWANA?
Sasa na litimie!"
16 Sijakukimbia na kuacha kuwa
mchungaji wako;
unajua sijaitamani siku ya kukata
tamaa.
Kile kipitacho midomoni mwangu
ki wazi mbele yako.
17 [c]Usiwe kwangu kitu cha kunitia hofu
kuu;
wewe ndiwe kimbilio langu katika
siku ya maafa.
18 [d]Watesi wangu na waaibishwe,
lakini nilinde mimi nisiaibike;
wao na watiwe hofu kuu,
lakini unilinde mimi na hofu kuu.
Waletee siku ya maafa;
waangamize kwa maangamizi
maradufu.

*Kuiadhimisha Sabato*

19 [e]Hili ndilo BWANA aliloniambia:
"Nenda ukasimame kwenye lango la watu,
mahali ambako wafalme wa Yuda huingilia
na kutokea, simama pia kwenye malango
mengine yote ya Yerusalemu. 20 [f]Waambie,
'Sikieni neno la BWANA, enyi wafalme wa
Yuda, nanyi watu wote wa Yuda, na kila
mmoja aishiye Yerusalemu apitaye katika
malango haya. 21 [g]Hili ndilo asemalo
BWANA: Jihadharini msije mkabeba mzigo
siku ya Sabato, wala kuingiza mzigo kupitia
malango ya Yerusalemu. 22 [h]Msitoe mizigo
nje ya nyumba zenu wala kufanya kazi
yoyote wakati wa Sabato, lakini itakaseni
siku ya Sabato, kama nilivyowaamuru
baba zenu. 23 [i]Hata hivyo hawakusikiliza
wala kujali, walishupaza shingo zao, na
hawakutaka kusikia wala kukubali adhabu.
24 Lakini mkiwa waangalifu kunitii, asema
BWANA, nanyi msipoleta mzigo wowote
kupitia malango ya mji huu wakati wa
Sabato, lakini mkaitakasa siku ya Sabato
kwa kutofanya kazi siku hiyo, 25 [j]ndipo
wafalme wakaao juu ya kiti cha enzi cha
Daudi wataingia kupitia malango ya mji
huu, pamoja na maafisa wao. Wao na
maafisa wao watakuja wakiwa wamepanda
magari na farasi, wakiandamana na watu
wa Yuda na wale waishio Yerusalemu,
nao mji huu utakaliwa na watu daima.
26 [k]Watu watakuja kutoka miji ya Yuda na
vijiji vinavyoizunguka Yerusalemu, kutoka
nchi ya Benyamini na chini ya vilima
vya magharibi, kutoka nchi ya vilima na
Negebu, wakileta sadaka za kuteketezwa
na dhabihu, sadaka za nafaka, uvumba na
sadaka za shukrani kwenye nyumba ya
BWANA. 27 [l]Lakini ikiwa hamtanitii mimi
kwa kuitakasa Sabato na kwa kutochukua
mzigo wowote mnapoingia katika malango
ya Yerusalemu wakati wa Sabato, basi
nitawasha moto usiozimika katika malango
ya Yerusalemu utakaoteketeza ngome
zake.' "

[a]**17:14** Kut 15:2; Isa 30:26; Yer 15:18; Za 109:1; 119:94
[b]**17:15** Isa 5:19; Amo 5:18; 2Pet 3:4-5
[c]**17:17** Za 88:15-16; 46:1; 18:18; Yer 16:19; Nah 1:7
[d]**17:18** Za 35:1-8; Isa 40:2; Yer 12:3
[e]**17:19** Yer 7:2; 26:2
[f]**17:20** Yer 19:3; 22:2; Za 49:1
[g]**17:21** Kum 5:14; Yn 5:10; Neh 13:15-21; Hes 15:32-36
[h]**17:22** Eze 20:12; Kut 20:8; Mwa 2:3; Isa 56:2-6
[i]**17:23** Yer 7:26; 19:15; 2Nya 28:22; Zek 7:11; Yer 7:28
[j]**17:25** 2Sam 7:13; Lk 1:32; Yer 22:2; 30:10; 33:19; Isa 6:6-7; Eze 28:26
[k]**17:26** Yer 33:14; Zek 7:7; Yer 32:44
[l]**17:27** Yer 22:5; 7:20; Hos 8:14; Amo 2:5; Neh 10:31; 2Fal 25:9; 1Fal 9:6

*Katika Nyumba Ya Mfinyanzi*

18 Hili ndilo neno lililomjia Yeremia
kutoka kwa BWANA: 2 “Shuka uende
mpaka nyumba ya mfinyanzi, nami
huko nitakupa ujumbe wangu.” 3 Kwa
hiyo nikashuka mpaka kwenye nyumba
ya mfinyanzi, nikamkuta akifinyanga
kwa gurudumu lake. 4 Lakini chombo
alichokuwa akikifinyanga kutokana na
udongo kilivunjika mikononi mwake,
hivyo mfinyanzi akakifanya kuwa
chombo kingine, umbo jingine kama vile
ilivyoonekana vyema kwake yeye.
5 Kisha neno la BWANA likanijia
kusema: 6 [a]“Ee nyumba ya Israeli, je,
siwezi kuwafanyia kama huyu mfinyanzi
afanyavyo?” asema BWANA. “Kama
vile udongo ulivyo katika mikono ya
mfinyanzi, ndivyo mlivyo katika mkono
wangu, ee nyumba ya Israeli. 7 [b]Ikiwa
wakati wowote nikitangaza kuwa taifa
au ufalme utang’olewa, utaangushwa na
kuangamizwa, 8 [c]ikiwa lile taifa nililolionya
litatubia uovu wake, ndipo nitakapokuwa
na huruma, wala sitawapiga kwa maafa
niliyokuwa nimewakusudia. 9 [d]Ikiwa
wakati mwingine nitatangaza kuwa taifa
ama utawala ujengwe na kuwekwa wakfu,
10 [e]ikiwa utafanya maovu mbele zangu na
hukunitii, ndipo nitakapoghairi makusudio
yangu mema niliyokuwa nimeyakusudia.
11 [f]“Basi kwa hiyo waambie watu wa Yuda
na wale waishio Yerusalemu, ‘Hili ndilo
asemalo BWANA: Tazama! Ninaandaa maafa
kwa ajili yenu, nami ninabuni mabaya dhidi
yenu. Kwa hiyo geukeni kutoka njia zenu
mbaya, kila mmoja wenu, tengenezeni
njia zenu na matendo yenu.’ 12 [g]Lakini wao
watajibu, ‘Hakuna faida. Tutaendelea na
mipango yetu wenyewe, kila mmoja wetu
atafuata ukaidi wa moyo wake mbaya.’ ”
13 [h]Kwa hiyo hili ndilo asemalo BWANA:

“Ulizia miongoni mwa mataifa:
Ni nani alishasikia jambo kama hili?
Jambo la kutisha sana limefanywa
na Bikira Israeli.
14 Je, barafu ya Lebanoni iliwahi kutoweka
kwenye miteremko yake ya mawe wakati wowote?
Je, maji yake baridi yatokayo katika vyanzo vilivyo mbali
yaliwahi kukoma kutiririka wakati wowote?
15 [i]Lakini watu wangu wamenisahau mimi,
wanafukizia uvumba sanamu zisizofaa kitu,
zilizowafanya wajikwae katika njia zao
na katika mapito ya zamani.
Zimewafanya wapite kwenye vichochoro
na kwenye barabara ambazo hazikujengwa.
16 [j]Nchi yao itaharibiwa,
itakuwa kitu cha kudharauliwa daima;
wote wapitao karibu nayo watashangaa
na kutikisa vichwa vyao.
17 [k]Kama upepo utokao mashariki,
nitawatawanya mbele ya adui zao;
nitawapa kisogo wala sio uso,
katika siku ya maafa yao.”

18 [l]Wakasema, “Njooni, tutunge hila
dhidi ya Yeremia; kwa kuwa kufundisha
sheria kwa kuhani hakutapotea, wala shauri

[a]**18:6** Isa 29:16; 45:9; Rum 9:20-21; Mwa 2:7
[b]**18:7** Yer 1:10
[c]**18:8** Kut 32:14; Eze 18:21; Yn 3:8-10; Dan 9:14; Amu 10:15-16; Za 25:11; Yer 26:13; 31:28; 42:10; Hos 11:8-9; Yoe 2:13
[d]**18:9** Yer 1:10; 31:28
[e]**18:10** Eze 33:18; 1Sam 2:29-30; 13:13; Yer 1:10
[f]**18:11** 2Fal 22:16; Yer 4:6; Kum 4:30; 2Fal 17:13; Isa 1:16-19; Ay 16:17; Yer 7:3
[g]**18:12** Isa 57:10; Yer 2:25; 3:17
[h]**18:13** Isa 66:8; Yer 2:10; 5:30; 2Fal 19:21
[i]**18:15** Yer 51:18; Hos 11:12; Yer 6:16; Isa 57:14; 62:10; 17:10; 1:13; Eze 44:12
[j]**18:16** Eze 33:28-29; Yer 49:13; 42:18; Ay 16:4; 2Fal 19:21; Kum 28:37; Yer 25:9
[k]**18:17** Ay 7:10; Yer 13:24; 2Nya 29:6; Yer 2:27
[l]**18:18** Yer 11:19; Hag 2:11; Yer 5:13; Za 64:2-8; Yer 9:3; 2:8; Mao 2:7; Ay 5:13

litokalo kwa mwenye hekima, wala neno la manabii. Hivyo njooni, tumshambulie kwa ndimi zetu na tusijali chochote asemacho."

19 Nisikilize, Ee Bwana,
sikia wanayosema washtaki wangu!
20 [a]Je, mema yalipwe kwa mabaya?
Lakini wao wamenichimbia shimo.
Kumbuka kwamba nilisimama mbele yako
na kunena mema kwa ajili yao,
ili wewe ugeuze hasira yako kali mbali nao.
21 [b]Kwa hiyo uwaache watoto wao waone njaa;
uwaache wauawe kwa makali ya upanga.
Wake zao wasiwe na watoto, na wawe wajane;
waume wao wauawe,
nao vijana wao waume
wachinjwe kwa upanga vitani.
22 [c]Kilio na kisikike kutoka kwenye nyumba zao
ghafula uwaletapo adui dhidi yao,
kwa kuwa wamechimba shimo ili kunikamata
na wameitegea miguu yangu mitego.
23 [d]Lakini unajua, Ee Bwana,
hila zao zote za kuniua.
Usiyasamehe makosa yao
wala usifute dhambi zao
mbele za macho yako.
Wao na waangamizwe mbele zako;
uwashughulikie wakati wa hasira yako.

*Gudulia La Udongo Lililovunjika*

19 [e]Hili ndilo asemalo Bwana: "Nenda
ukanunue gudulia la udongo kutoka
kwa mfinyanzi. Wachukue baadhi ya
wazee wa watu na wa makuhani 2 [f]na
mtoke mwende mpaka kwenye Bonde
la Ben-Hinomu, karibu na ingilio la
Lango la Vigae. Huko tangaza maneno
ninayokuambia, 3 [g]nawe useme, 'Sikieni
neno la Bwana, enyi wafalme wa Yuda
na watu wa Yerusalemu. Hili ndilo Bwana
Mwenye Nguvu Zote, Mungu wa Israeli,
asemalo: Sikilizeni! Nitaleta maafa mahali
hapa, ambayo yatafanya masikio ya kila
mmoja atakayesikia habari zake yawashe.
4 [h]Kwa kuwa wameniacha na kupafanya
mahali hapa kuwa pa miungu ya kigeni.
Wameiteketezea sadaka miungu ambayo
wao wala baba zao wala wafalme wa
Yuda kamwe hawakuijua, nao wamelijaza
eneo hili kwa damu isiyo na hatia.
5 [i]Wamejenga mahali pa juu pa kuabudia
miungu pa Baali ili kuteketeza wana wao
katika moto kama sadaka kwa Baali, kitu
ambacho sikukiamuru wala kukitaja, wala
hakikuingia akilini mwangu. 6 [j]Hivyo
jihadharini, siku zinakuja, asema Bwana,
wakati watu hawatapaita tena mahali hapa
Tofethi ama Bonde la Ben-Hinomu, bali
Bonde la Machinjo.
7 [k]" 'Nitaiharibu mipango ya Yuda na
Yerusalemu mahali hapa. Nitawafanya
waanguke kwa upanga mbele ya adui zao,
katika mikono ya wale watafutao uhai wao,
nami nitaitoa mizoga yao kuwa chakula
cha ndege wa angani na wanyama wa nchi.
8 [l]Nitauharibu mji huu na kuufanya kitu
cha kudharauliwa. Wote wapitao karibu
watashangaa na kuudhihaki kwa sababu
ya majeraha yake yote. 9 [m]Nitawafanya
wao kula nyama ya wana wao na binti zao;

[a]**18:20** Mwa 20:7; Kum 9:19; Za 119:85; 35:7; 109:23; Mwa 44:4; Yer 14:7-9
[b]**18:21** Yer 11:22; 14:16; 1Sam 15:33; Mao 5:3; Za 63:10; Isa 47:9; 9:17
[c]**18:22** Yer 6:26; Za 35:15; Yer 5:26; Za 119:85; Yer 20:10
[d]**18:23** Yer 11:21; 37:15; Neh 4:5; Za 109:14; 59:5; Yer 10:24
[e]**19:1** Hes 11:17; Yer 18:2
[f]**19:2** Yos 15:8; 2Fal 23:10
[g]**19:3** Yer 17:20; 6:19; 1Sam 3:11
[h]**19:4** Kum 28:20; 31:16; Law 18:21; 2Fal 21:16; Isa 65:11; Kut 20:3; Yer 1:16
[i]**19:5** 2Fal 3:27; Za 106:37-38; Yer 32:35; Eze 16:36; Yer 7:31
[j]**19:6** Yos 15:8; Yer 7:32; 2Fal 23:10
[k]**19:7** Law 26:17; Kum 28:25-26; Yer 16:4; Za 79:2; 33:10-11; Yer 34:20
[l]**19:8** Kum 28:37; Yer 25:9; Mao 2:15-16; Sef 2:15; Yer 18:16; Law 26:32
[m]**19:9** Law 26:29; Mao 4:10; Isa 9:20; Kum 28:49-57; Yer 21:7

kila mmoja atakula nyama ya mwenzake
wakati wa dhiki ya kuzungukwa na jeshi
lililowekwa juu yao na adui wanaotafuta
uhai wao.'
10 [a]"Kisha livunje lile gudulia wale
walio pamoja nawe wakiwa wanaangalia,
11 [b]uwaambie, 'Hili ndilo BWANA Mwenye
Nguvu Zote asemalo: Nitalivunja taifa
hili na mji huu kama gudulia hili la
mfinyanzi lilivyovunjwa, nalo haliwezi
kutengenezeka tena. Watawazika waliokufa
huko Tofethi hata isiwepo nafasi zaidi.
12 Hivi ndivyo nitakavyopafanya mahali
hapa na kwa wale waishio ndani yake,
asema BWANA. Nitaufanya mji huu kama
Tofethi. 13 [c]Nyumba zilizoko Yerusalemu na
zile za wafalme wa Yuda zitatiwa unajisi
kama mahali hapa, Tofethi: yaani nyumba
zote ambazo walifukiza uvumba juu ya
mapaa yake kwa jeshi lote la angani, na
kumimina dhabihu za vinywaji kwa miungu
mingine.' "
14 [d]Kisha Yeremia akarudi kutoka Tofethi,
mahali ambapo BWANA alikuwa amemtuma
kutoa unabii, akasimama katika ua wa
Hekalu la BWANA na kuwaambia watu
wote, 15 [e]"Hili ndilo BWANA Mwenye Nguvu
Zote, Mungu wa Israeli, asemalo: 'Sikilizeni!
Nitaleta juu ya mji huu pamoja na vijiji
vinavyouzunguka kila maafa niliyosema
dhidi yake, kwa sababu wamekuwa na
shingo ngumu, na hawakuyasikiliza maneno
yangu.' "

*Yeremia Ateswa Na Pashuri*

20 [f]Ikawa kuhani Pashuri mwana wa
Imeri, mkuu wa maafisa wa Hekalu
la BWANA, alipomsikia Yeremia akitoa
unabii juu ya mambo haya, 2 [g]akaamuru
Yeremia nabii apigwe na kufungwa kwenye
mkatale katika Lango la Juu la Benyamini
huko Hekaluni la BWANA. 3 Siku ya pili
Pashuri alipomwachia kutoka kwenye
mkatale, Yeremia akamwambia, "BWANA
hakukuita jina lako kuwa Pashuri bali
Magor-Misabibu.[h] 4 [i]Kwa kuwa hili ndilo
asemalo BWANA: 'Nitakufanya kuwa hofu
kuu kwako wewe mwenyewe na rafiki
zako wote, na kwa macho yako mwenyewe
utawaona wakianguka kwa upanga wa adui
zao. Nitawatia Yuda wote mikononi mwa
mfalme wa Babeli, ambaye atawachukua
na kuwapeleka Babeli, ama awaue kwa
upanga. 5 [j]Nitatia utajiri wote wa mji huu
kwa adui zao: yaani mazao yao yote, vitu
vyao vyote vya thamani, na hazina zote za
wafalme wa Yuda. Watavitwaa kwa nyara
na kuvipeleka Babeli. 6 [k]Nawe Pashuri
pamoja na wote waishio katika nyumba
yako mtakwenda uhamishoni Babeli. Mtafia
humo na kuzikwa, wewe na rafiki zako
wote ambao umewatabiria uongo.' "

*Malalamiko Ya Yeremia*

7 [l]Ee BWANA, umenidanganya,
nami nikadanganyika;
wewe una nguvu kuniliko,
nawe umenishinda.
Ninadharauliwa mchana kutwa,
kila mmoja ananidhihaki.
8 [m]Kila ninenapo, ninapiga kelele
nikitangaza ukatili na uharibifu.
Kwa hiyo neno la BWANA
limeniletea matukano
na mashutumu mchana kutwa.
9 [n]Lakini kama nikisema, "Sitamtaja
wala kusema tena kwa jina lake,"

---

[a]**19:10** Yer 13:14; 51:63; Za 2:9
[b]**19:11** Yer 7:32; Za 2:9; Isa 30:14
[c]**19:13** Yer 52:13; Eze 16:41; Ay 38:32; Mdo 7:42; Eze 20:28; Yer 7:18; 32:29; Eze 20:28
[d]**19:14** 2Nya 20:5; Yer 7:2; 26:2
[e]**19:15** Zek 7:11-14; Mdo 7:51-52; Neh 9:16; Yer 11:11; 22:21
[f]**20:1** 1Nya 24:14; 2Fal 25:18; Lk 22:52
[g]**20:2** Kum 25:2-3; 2Kor 11:24; Ay 13:27; Zek 14:10; Ay 29:7; Yer 15:15; 37:15; 29:26; Mdo 16:24; Ebr 11:36

[h]3 Magor-Misabibu maana yake hapa ni Vitisho pande zote.
[i]**20:4** Ay 18:11; Yer 29:21; 25:9; 52:27; 39:9; 21:10; 13:19
[j]**20:5** 2Fal 25:15; Yer 17:3; 3:24; 2Fal 20:17
[k]**20:6** Yer 14:15; Mao 2:14; Yer 28:15
[l]**20:7** Kut 5:23; 22:16; Isa 8:11; 1Kor 9:16; Ay 12:4
[m]**20:8** Yer 28:8; 2Nya 36:16; Yer 6:7-10
[n]**20:9** Za 39:3; Yer 4:19; Amo 3:8; Mdo 4:20; 18:5; Yer 44:16

neno lake linawaka ndani ya moyo
wangu kama moto,
moto uliofungwa ndani ya mifupa
yangu.
Nimechoka sana kwa kulizuia ndani
mwangu;
kweli, siwezi kujizuia.
10 [a]Ninasikia minong'ono mingi,
"Hofu iko pande zote!
Mshtakini! Twendeni tumshtaki!"
Rafiki zangu wote wananisubiri
niteleze,
wakisema,
"Labda atadanganyika;
kisha tutamshinda
na kulipiza kisasi juu yake."

11 [b]Lakini BWANA yu pamoja nami
kama shujaa mwenye nguvu;
hivyo washtaki wangu watajikwaa
na kamwe hawatashinda.
Watashindwa, nao wataaibika
kabisa;
kukosa adabu kwao
hakutasahauliwa.
12 [c]Ee BWANA Mwenye Nguvu Zote,
wewe umjaribuye mwenye haki
na kupima moyo na nia,
hebu nione ukilipiza kisasi juu yao,
kwa maana kwako
nimeliweka shauri langu.

13 [d]Mwimbieni BWANA!
Mpeni BWANA sifa!
Yeye huokoa uhai wa mhitaji
kutoka mikononi mwa waovu.

14 [e]Ilaaniwe siku niliyozaliwa!
Nayo isibarikiwe ile siku
mama yangu aliyonizaa!

15 Alaaniwe mtu yule aliyemletea baba
yangu habari,
yule aliyemfanya afurahi sana,
akisema,
"Mtoto amezaliwa kwako,
tena mtoto wa kiume!"
16 [f]Mtu huyo na awe kama miji ile
ambayo BWANA Mungu
aliiangamiza bila huruma.
Yeye na asikie maombolezo asubuhi
na kilio cha vita adhuhuri.
17 [g]Kwa sababu hakuniua nikiwa
tumboni,
hivyo mama yangu angekuwa
kaburi langu,
nalo tumbo lake la uzazi
lingebaki kuwa kubwa daima.
18 [h]Kwa nini basi nilitoka tumboni
ili kuona taabu na huzuni,
na kuzimaliza siku zangu katika
aibu?

*Mungu Anakataa Ombi La Sedekia*

21 [i]Neno lilimjia Yeremia kutoka kwa
BWANA wakati Mfalme Sedekia
alipowatuma Pashuri mwana wa Malkiya,
na kuhani Sefania mwana wa Maaseya
kwake, kusema: 2 [j]"Tuulizie sasa kwa
BWANA, kwa sababu Nebukadneza
mfalme wa Babeli anatushambulia. Labda
BWANA atatenda maajabu kwa ajili yetu
kama nyakati zilizopita, ili Nebukadneza
atuondokee."
3 Lakini Yeremia akawajibu, "Mwambieni
Sedekia, 4 [k]'Hili ndilo BWANA, Mungu wa
Israeli, asemalo: Ninakaribia kuwageuzia
silaha za vita zilizo mikononi mwenu,
ambazo mnatumia kupigana na mfalme
wa Babeli na Wakaldayo ambao wako nje
ya ukuta wakiwazunguka kwa jeshi. Nami

[a]**20:10** Yer 6:25; Neh 6:6-13; Ay 19:14; Lk 11:54; Za 57:4
[b]**20:11** Rum 8:31; Yer 15:15; 17:18; 23:40; 7:19; Za 129:2
[c]**20:12** Yer 17:10; Za 54:7; Rum 12:19; Za 62:8; Yer 11:20; Za 7:9; Kum 32:35
[d]**20:13** Za 35:10; Yak 2:5-6; Isa 12:6; Za 34:6; 97:10
[e]**20:14** Yer 15:10; Ay 3:8, 16
[f]**20:16** Mwa 19:25; Yer 18:22; 6:26
[g]**20:17** Ay 3:10-16; 10:18-19
[h]**20:18** 1Fal 19:4; Za 102:3; Ay 3:20; 3:10-11; Mhu 4:2; Mwa 3:17; Ay 5:7; Za 90:9
[i]**21:1** 2Fal 24:18; 1Nya 9:12; 2Fal 25:18; Yer 37:3; 52:1
[j]**21:2** Mwa 25:22; Yer 32:5; Za 44:1-4; Yer 32:17; Kut 9:28; 2Fal 22:18; Mwa 10:10
[k]**21:4** Yer 32:5; 37:8-10; Isa 13:4

nitawakusanya ndani ya mji huu. 5 [a]Mimi
mwenyewe nitapigana dhidi yenu kwa
mkono wangu ulionyooshwa na mkono
wa nguvu, kwa hasira na ghadhabu kali na
ukali mwingi. 6 [b]Nitawaangamiza waishio
katika mji huu, watu na wanyama, nao
watauawa kwa tauni ya kutisha. 7 [c]Baada
ya hayo, nitamtia Sedekia mfalme wa
Yuda, maafisa wake na watu wa mji huu
ambao walinusurika tauni, upanga na njaa,
mkononi mwa Nebukadneza mfalme wa
Babeli, na kwa adui zao wale wanaotafuta
uhai wao. Atawaua kwa upanga; hatakuwa
na rehema juu yao au huruma wala
kuwasikitikia,' asema BWANA.
8 "Zaidi ya hayo, waambie watu hawa,
'Hili ndilo asemalo BWANA: Tazama,
naweka mbele yenu njia ya uzima, na njia
ya mauti. 9 [d]Yeyote atakayekaa katika mji
huu atakufa kwa upanga, njaa au tauni.
Lakini yeyote atakayetoka na kujisalimisha
kwa Wakaldayo ambao wameuzunguka mji
huu kwa jeshi, atanusurika, naye ataishi.
10 [e]Nimekusudia kuufanyia mji huu jambo
baya, wala si jema. Utatiwa mikononi mwa
mfalme wa Babeli, naye atauteketeza kwa
moto, asema BWANA.'
11 [f]"Zaidi ya hayo, ambia nyumba ya
mfalme ya Yuda, 'Sikia neno la BWANA,
12 [g]Ewe nyumba ya Daudi, hili ndilo BWANA
asemalo:

" 'Hukumuni kwa haki kila asubuhi,
mwokoeni mikononi mwa
mdhalimu
yeye aliyetekwa nyara,
la sivyo ghadhabu yangu italipuka
na kuwaka kama moto
kwa sababu ya uovu mlioufanya:
itawaka na hakuna wa kuizima.

13 [h]Niko kinyume nawe, ee Yerusalemu,
wewe uishiye juu ya bonde hili
kwenye uwanda wa juu wa
miamba,
asema BWANA,
wewe usemaye, "Ni nani awezaye
kuja kinyume chetu?
Nani ataingia mahali pa kimbilio
letu?"
14 [i]Nitawaadhibu kama istahilivyo
matendo yenu,
asema BWANA.
Nitawasha moto katika misitu yenu
ambao utateketeza kila kitu
kinachowazunguka.' "

*Hukumu Dhidi Ya Wafalme Waovu*

22 Hili ndilo asemalo BWANA: "Shuka
kwenye jumba la kifalme la mfalme
wa Yuda, utangaze ujumbe huu huko:
2 [j]'Sikia neno la BWANA, ee mfalme wa
Yuda, wewe uketiye kwenye kiti cha enzi
cha Daudi: wewe, maafisa wako na watu
wako mnaopitia malango haya. 3 [k]Hili
ndilo BWANA asemalo: Tenda haki na
adili. Mwokoe mkononi mwa mdhalimu
yeye aliyetekwa nyara. Usimtendee mabaya
wala ukatili mgeni, yatima au mjane, wala
usimwage damu isiyo na hatia mahali hapa.
4 [l]Kwa kuwa ukiwa mwangalifu kushika
maagizo haya, ndipo wafalme watakaokalia
kiti cha enzi cha Daudi watakapoingia
kupitia malango ya jumba hili la kifalme,
wakiwa wamepanda magari na farasi, huku
wakifuatana na maafisa wao na watu wao.
5 [m]Lakini kama hutayatii maagizo haya,
asema BWANA, ninaapa kwa nafsi yangu
kwamba jumba hili litakuwa gofu.' "
6 [n]Kwa kuwa hili ndilo BWANA asemalo

---

[a]**21:5** 2Fal 22:13; Yer 6:12; Kut 6:6; 3:20; Yos 10:14; Eze 5:8
[b]**21:6** Yer 14:12; 7:20
[c]**21:7** Eze 12:14; 2Nya 36:10; Eze 29:19; Hab 1:6; Yer 39:5; 2Fal 25:7; Yer 52:9; 27:6
[d]**21:9** Yer 14:12; Eze 5:12; Yer 39:18; 45:5; 27:11; 40:9; 39:18
[e]**21:10** Yer 20:4; Amo 9:4; Yer 22:3; Isa 1:31; 42:25
[f]**21:11** Yer 13:18
[g]**21:12** Kut 22:22; Yer 22:3; Isa 1:31; 42:25
[h]**21:13** Nah 2:13; Eze 5:8; 2Sam 5:6-7; Oba 1:3-4; Yer 49:4; 23:30; 50:31; 51:25
[i]**21:14** Mit 1:31; Isa 3:10-11; 2Nya 36:19; 2Fal 19:23; Mao 2:3; Eze 20:47; Yer 17:10
[j]**22:2** Lk 1:32; Amo 7:16
[k]**22:3** Law 25:17; Hos 12:6; Yer 21:12; Za 72:4; Isa 1:17; Amo 5:24; Eze 33:14; Mik 6:8
[l]**22:4** Yer 17:25
[m]**22:5** Yer 17:25; Mwa 22:16; Ebr 6:13
[n]**22:6** Mik 3:12; Mwa 31:21; Wim 4:1; Isa 33:9; 1Fal 7:2

kuhusu jumba la kifalme la mfalme wa Yuda:

"Ingawa uko kama Gileadi kwangu,
kama kilele cha Lebanoni,
hakika nitakufanya uwe kama jangwa,
kama miji ambayo haijakaliwa na watu.
7 [a]Nitawatuma waharabu dhidi yako,
kila mtu akiwa na silaha zake,
nao watazikata boriti zako nzuri za mierezi
na kuzitupa motoni.

8 [b]"Watu kutoka mataifa mengi watapitia
karibu na mji huu na kuulizana, 'Kwa nini
BWANA amefanya jambo la namna hii juu
ya mji huu mkubwa?' 9 [c]Nalo jibu litakuwa:
'Kwa sababu wameliacha agano la BWANA,
Mungu wao, na wameabudu na kuitumikia
miungu mingine.' "

10 [d]Usimlilie yeye aliyekufa, wala usimwombolezee;
badala yake, afadhali umlilie kwa uchungu
yule aliyepelekwa uhamishoni,
kwa sababu kamwe hatairudia
wala kuiona tena nchi yake alikozaliwa.

11 [e]Kwa kuwa hili ndilo asemalo BWANA
kuhusu Shalumu[f] mwana wa Yosia,
aliyeingia mahali pa baba yake kuwa
mfalme wa Yuda, lakini ameondoka mahali
hapa: "Yeye kamwe hatarudi tena. 12 [g]Atafia
huko mahali walipompeleka kuwa mateka;
hataiona tena nchi hii."

13 [h]"Ole wake yeye ajengaye jumba lake la kifalme kwa njia ya dhuluma,
vyumba vyake vya juu kwa udhalimu,
akiwatumikisha watu wa nchi yake pasipo malipo,
bila kuwalipa kwa utumishi wao.
14 [i]Asema, 'Nitajijengea jumba kuu la kifalme,
na vyumba vya juu vyenye nafasi kubwa.'
Hivyo anaweka ndani yake madirisha makubwa,
huweka kuta za mbao za mierezi,
na kuipamba kwa rangi nyekundu.

15 [j]"Je, inakufanya kuwa mfalme
huko kuongeza idadi ya mierezi?
Je, baba yako hakuwa na chakula na kinywaji?
Alifanya yaliyo sawa na haki,
hivyo yeye akafanikiwa katika yote.
16 [k]Aliwatetea maskini na wahitaji,
hivyo yeye akafanikiwa katika yote.
Je, hiyo si ndiyo maana ya kunijua mimi?"
asema BWANA.
17 [l]"Lakini macho yako na moyo wako vimeelekezwa tu
katika mapato ya udhalimu,
kwa kumwaga damu isiyo na hatia,
kwa uonevu na ukatili."

18 Kwa hiyo hili ndilo asemalo BWANA
kuhusu Yehoyakimu mwana wa Yosia
mfalme wa Yuda:

"Hawatamwombolezea wakisema:
'Ole, ndugu yangu! Ole, umbu langu!'

---

[a]**22:7** Yer 6:4; Isa 10:34; Za 74:5; Isa 21:14; Yer 4:7; Zek 11:1; 2Nya 36:16
[b]**22:8** Kum 29:24-26; 1Fal 9:8-9; Yer 16:10-11
[c]**22:9** 2Fal 22:17; Yer 16:11; Eze 39:23; 1Fal 9:9
[d]**22:10** Mhu 4:2; Eze 24; 16; Yer 24:9; 29:18; 42:18
[e]**22:11** 2Fal 23:30-31; 1Nya 3:15
[f]11 Shalumu ndiye pia anaitwa Yehoahazi.
[g]**22:12** 2Fal 23:34
[h]**22:13** Mik 3:10; Hab 2:9; Law 19:13; Yak 5:4; Isa 5:8
[i]**22:14** Isa 5:8-9; 2Sam 7:2; Eze 23:14
[j]**22:15** 2Fal 23:25; Za 22:21; Kum 9:7; Yer 3:13; Sef 3:2; Isa 3:10; Za 128:2
[k]**22:16** Za 72:1-4, 12-13; Yn 8:19; Tit 1:16; Yak 1:22; Za 82:3; Mit 24:23
[l]**22:17** Eze 19:6; 2Fal 24:4; Isa 56:11; Eze 18:12; Mik 2:2; Kum 28:33

Hawatamwombolezea wakisema:
‘Ole, bwana wangu! Ole, fahari
yake!’
19 [a]Atazikwa maziko ya punda:
ataburutwa na kutupwa
nje ya malango ya Yerusalemu.”

20 [b]“Panda Lebanoni ukapige kelele,
sauti yako na isikike huko
Bashani,
piga kelele toka Abarimu,
kwa kuwa wote waliojiunga nawe
wameangamizwa.
21 [c]Nilikuonya wakati ulipojisikia
kwamba uko salama,
lakini ulisema, ‘Mimi sitasikiliza!’
Hii imekuwa kawaida yako tangu
ujana wako;
hujanitii mimi.
22 [d]Upepo utawaondoa wachungaji
wako wote,
na wale ulioungana nao wataenda
uhamishoni.
Kisha utaaibika na kufedheheka
kwa sababu ya uovu wako wote.
23 Wewe uishiye Lebanoni,
wewe uliyetulia kwenye majengo
ya mierezi,
tazama jinsi utakavyoomboleza
maumivu makali yatakapokupata,
maumivu kama yale ya mwanamke
mwenye utungu wa kuzaa!

24 [e]“Hakika kama niishivyo,” asema
Bwana, “hata kama wewe, Yekonia[f]
mwana wa Yehoyakimu mfalme wa
Yuda, ungekuwa pete yangu ya muhuri
katika mkono wangu wa kuume, bado
ningekung’oa hapo. 25 [g]Nitakutia mikononi
mwa wale wanaotafuta uhai wako, wale
unaowaogopa, yaani Nebukadneza mfalme
wa Babeli na kwa Wakaldayo. 26 [h]Nitakutupa
mbali wewe na mama aliyekuzaa mwende
katika nchi nyingine, ambayo hakuna
hata mmoja wenu aliyezaliwa huko, nanyi
mtafia huko. 27 Kamwe hamtarudi katika
nchi mliyotamani kuirudia.”

28 [i]Je, huyu mtu Yekonia ni chungu
kilichodharauliwa,
chungu kilichovunjika,
chombo kisichotakiwa na mtu
yeyote?
Kwa nini yeye na watoto wake
watupwe nje kwa nguvu,
na kutupwa kwenye nchi
wasioijua?
29 [j]Ee nchi, nchi, nchi,
sikia neno la Bwana!
30 [k]Hili ndilo Bwana asemalo:
“Mwandike huyu mtu kama asiye na
mtoto,
mtu ambaye hatafanikiwa maisha
yake yote,
kwa maana hakuna mtoto wake
atakayefanikiwa,
wala kukaa kwenye kiti cha enzi
cha Daudi
wala kuendelea kutawala katika
Yuda.”

### *Tawi La Haki*

23 [l]“Ole wao wachungaji wanaoharibu na
kutawanya kondoo wa malisho yangu!”
asema Bwana. 2 [m]Kwa hiyo hili ndilo
Bwana, Mungu wa Israeli, analowaambia
wachungaji wanaowachunga watu wangu:
“Kwa sababu mmelitawanya kundi langu na
kuwafukuzia mbali, wala hamkuwatunza,
basi mimi nitawaadhibu kwa ajili ya

[a]**22:19** 2Fal 24:6; Yer 36:30
[b]**22:20** Hes 27:12; Isa 57:13; Za 68:15; Yer 30:14; Eze 16:33-34; Hos 8:9
[c]**22:21** Yer 3:25; 3:13; Sef 3:2; Za 25:7; Zek 7:7; Kum 9:7; Isa 54:4; Yer 7:23-28
[d]**22:22** Yer 7:19; 10:21; Ay 27:21
[e]**22:24** 2Fal 24:6-8; Yer 37:1; Hag 2:23; Mwa 38:18
[f]24 Yekonia au Konia ni jina jingine la Yehoyakini.
[g]**22:25** 2Fal 24:16; 2Nya 36:10; Yer 34:20
[h]**22:26** 1Sam 25:29; Isa 22:17; Eze 19:9-14; 1Fal 2:19; 2Fal 24:8; 2Nya 36:10
[i]**22:28** Za 31:12; Hos 8:8; Yer 17:4; 48:38; 2Fal 24:6; Yer 19:10
[j]**22:29** Yer 6:19
[k]**22:30** 1Nya 3:16-18; Mt 1:12; Yer 10:21; 38:23; 52:10; Ay 18:19; Za 94:20
[l]**23:1** Eze 34:1-10; Zek 11:5-7, 15-17; Isa 56:11; Eze 34:31; Yer 10:21; 12:10; 25:36
[m]**23:2** Kut 32:34; Yer 21:12; Eze 34:8-10; Yn 10:8; Yer 10:21; 13:20

uovu mliofanya," asema BWANA.
3 [a]"Mimi mwenyewe nitayakusanya mabaki ya kundi langu kutoka nchi zote ambazo nimewafukuzia, nami nitawarudisha katika malisho yao, mahali ambapo watazaa na kuongezeka idadi yao.
4 [b]Nitaweka wachungaji juu yao ambao watawachunga, nao hawataogopa tena au kutishwa, wala hatapotea hata mmoja," asema BWANA.

5 [c]BWANA asema, "Siku zinakuja,
nitakapomwinulia Daudi Tawi
lenye haki,
Mfalme atakayetawala kwa hekima,
na kutenda lililo haki na sawa
katika nchi.
6 [d]Katika siku zake, Yuda ataokolewa
na Israeli ataishi salama.
Hili ndilo jina atakaloitwa:
BWANA Haki Yetu.

7 [e]"Hivyo basi, siku zinakuja, wakati ambapo watu hawatasema tena, 'Hakika kama BWANA aishivyo, aliyewapandisha Waisraeli kutoka Misri,'
8 [f]bali watasema, 'Hakika kama BWANA aishivyo, aliyewatoa wazao wa Israeli kutoka nchi ya kaskazini na nchi zote alizokuwa amewafukuzia,' asema BWANA. Ndipo wataishi katika nchi yao wenyewe."

*Manabii Wasemao Uongo*

9 [g]Kuhusu manabii:

Moyo wangu umevunjika ndani
yangu;
mifupa yangu yote inatetemeka.
Nimekuwa kama mtu aliyelewa,
kama mtu aliyelemewa na divai,
kwa sababu ya BWANA
na maneno yake matakatifu.
10 [h]Nchi imejaa wazinzi;
kwa sababu ya laana, nchi
imekauka
na malisho yaliyoko nyikani
yamekauka.
Mwenendo wa manabii ni mbaya
na mamlaka yao si ya haki.

11 [i]"Nabii na kuhani wote si wacha
Mungu;
hata hekaluni mwangu ninaona
uovu wao,"
asema BWANA.
12 [j]"Kwa hiyo mapito yao yatakuwa
utelezi,
watafukuziwa mbali gizani
na huko wataanguka.
Nitaleta maafa juu yao
katika mwaka wa kuadhibiwa
kwao,"
asema BWANA.

13 [k]"Miongoni mwa manabii wa
Samaria
nililiona jambo la kuchukiza:
Walitabiri kwa Baali
na kuwapotosha Israeli watu
wangu.
14 [l]Nako miongoni mwa manabii wa
Yerusalemu
nimeona jambo baya sana:
Wanafanya uzinzi
na kuenenda katika uongo.
Wanatia nguvu mikono ya watenda
mabaya,
kwa ajili hiyo hakuna yeyote
anayeachana na uovu wake.

---

[a]**23:3** Isa 11:10-12; Eze 34:11-16; Yer 32:37; 1Fal 8:48
[b]**23:4** Mwa 48:15; Isa 31:4; Yer 46:26-28; Yn 6:39; Yer 30:10; 31:10
[c]**23:5** 2Fal 19:26; Eze 17:22; Mwa 18:19; Zek 6:12; Dan 9:24; Isa 4:2
[d]**23:6** Kut 23:21; Ezr 9:15; Zek 14:11; 1Kor 1:30; Law 25:18; Kum 32:8; Hos 2:8; Yer 33:16; Rum 3:21-22; Isa 42:6
[e]**23:7** Kum 15:15; Yer 16:14; 30:3
[f]**23:8** Eze 34:13; Isa 43:5-6; Yer 30:10; Eze 20:42; Amo 9:14-15
[g]**23:9** Hab 3:16; Yer 20:8-9; 4:19; Ay 4:14
[h]**23:10** Za 107:34; Yer 9:2, 10; 4:26; Hos 4:2-3; Kum 28:23-24; Yer 12:11
[i]**23:11** Yer 6:13; Sef 3:4; 2Fal 21:4; Yer 8:10; 7:10
[j]**23:12** Ay 3:23; Za 35:6; Mit 4:19; Yer 11:23; Kum 32:35; Yer 13:16
[k]**23:13** 1Fal 18:18-22; Isa 9:16; 3:12; Eze 13:10
[l]**23:14** Yer 5:30; Hos 6:10; Yer 29:23; Eze 13:22; Mt 11:24; Isa 1:9-10; Amo 4:11; Isa 5:18

Wote wako kama Sodoma kwangu;
watu na Yerusalemu wako kama
Gomora."

15 [a]Kwa hiyo, hili ndilo BWANA Mwenye Nguvu Zote asemalo kuhusu manabii:

"Nitawafanya wale chakula kichungu
na kunywa maji yaliyotiwa sumu,
kwa sababu kutokana na manabii wa
Yerusalemu
kutokumcha Mungu kumeenea
katika nchi yote."

16 [b]Hili ndilo BWANA Mwenye Nguvu Zote asemalo:

"Msisikilize wanachowatabiria
manabii,
wanawajaza matumaini ya uongo.
Wanasema maono kutoka akili zao
wenyewe,
hayatoki katika kinywa cha
BWANA.
17 [c]Huendelea kuwaambia wale
wanaonidharau mimi,
'BWANA asema: Mtakuwa na
amani.'
Kwa wale wote wafuatao ugumu wa
mioyo yao,
wao husema, 'Hakuna dhara
litakalowapata.'
18 [d]Lakini ni yupi miongoni mwao
aliyesimama katika baraza la
BWANA
ili kuona au kusikia neno lake?
Ni nani aliyesikiliza
na kusikia neno lake?
19 [e]Tazama, dhoruba ya BWANA
itapasuka kwa ghadhabu,
kisulisuli kitazunguka na kuanguka
vichwani vya waovu.
20 [f]Hasira ya BWANA haitageuka mpaka
amelitimiza kusudi la moyo
wake.
Siku zijazo mtalifahamu kwa wazi.
21 [g]Mimi sikuwatuma manabii hawa,
lakini bado wamekimbia
wakitangaza ujumbe wao.
Mimi sikusema nao,
lakini wametabiri.
22 [h]Lakini kama wangesimama barazani
mwangu,
wangetangaza maneno yangu kwa
watu wangu,
nao wangewageuza kutoka njia zao
mbaya
na kutoka matendo yao maovu."
23 [i]"Je, mimi ni Mungu aliyeko hapa
karibu tu,"
BWANA asema,
"wala si Mungu aliyeko pia mbali?
24 [j]Je, mtu yeyote aweza kujificha
mahali pa siri ili nisiweze
kumwona?"
BWANA asema.
"Je, mimi sikuijaza mbingu na
nchi?"
BWANA asema.

25 [k]"Nimesikia wanayoyasema manabii,
hao wanaotabiri uongo kwa jina langu.
Wanasema, 'Nimeota ndoto! Nimeota
ndoto!' 26 [l]Mambo haya yataendelea mpaka
lini ndani ya mioyo ya hawa manabii wa
uongo, ambao hutabiri maono ya uongo ya
akili zao wenyewe? 27 [m]Wanadhani ndoto
wanazoambiana wao kwa wao zitawafanya
watu wangu walisahau jina langu, kama
baba zao walivyolisahau jina langu kwa
kumwabudu Baali. 28 [n]Mwache nabii aliye

[a]**23:15** Yer 8:14; 9:15; 8:10
[b]**23:16** Yer 27:9-14; Mt 7:15; Mit 19:27; Eze 13:3; Yer 14:14; 9:20
[c]**23:17** Yer 13:10; 8:11; Amo 9:10; Mik 3:11; 1Fal 22:8; Yer 4:10; 5:12
[d]**23:18** 1Fal 22:19; Rum 11:34
[e]**23:19** Isa 30:30; Yer 30:23; 25:32; Zek 7:14
[f]**23:20** 2Fal 23:26-27; Yer 30:24; 4:28
[g]**23:21** Yer 14:14; 27:15
[h]**23:22** 2Fal 17:13; Kum 33:10; 2Fal 17:13; Yer 25:5; Amo 3:7
[i]**23:23** Za 139:1-10; 1Fal 20:23-28
[j]**23:24** Ay 11:20; 1Fal 8:27; Ebr 4:13; Mwa 3:8; Ay 22:12-14; Mhu 12:14; Isa 28:15; 1Kor 4:5
[k]**23:25** Yer 14:14; 27:10; 29:8; Kum 13:1
[l]**23:26** Isa 30:10; 1Tim 4:1-2; Eze 13:2; Yer 14:14
[m]**23:27** Kum 13:13; Yer 29:8; Amu 3:7; 8:33-34; Mdo 13:8; Yer 2:23
[n]**23:28** 1Sam 3:17

na ndoto aseme ndoto yake, lakini yule aliye
na neno langu na aliseme kwa uaminifu.
Kwa maana jani kavu lina uhusiano gani
na ngano?” asema BWANA. 29 [a]“Je, neno
langu si kama moto,” asema BWANA, “na
kama nyundo ivunjayo mwamba vipande
vipande?

30 [b]“Kwa hiyo, niko kinyume na manabii
wanaoibiana maneno kana kwamba ni
yangu,” asema BWANA. 31 “Naam, mimi
niko kinyume na manabii wanaotikisa
ndimi zao wenyewe na kusema, ‘BWANA
asema.’ 32 [c]Kweli, niko kinyume na hao
wanaotabiri ndoto za uongo,” asema
BWANA. “Wanazisimulia na kuwapotosha
watu wangu kwa uongo wao bila kujali,
lakini sikuwatuma wala sikuwaamuru.
Hawawafaidi watu hawa hata kidogo,”
asema BWANA.

*Maneno Ya Uongo Na Manabii Wa Uongo*

33 [d]“Wakati watu hawa, au nabii, au
kuhani watakapokuuliza, ‘Mzigo wa
BWANA ni nini?’ wewe utawaambia,
‘Ninyi ndio mzigo. Nami nitawavua kama
vazi, asema BWANA.’ 34 [e]Nabii, kuhani, au
mtu yeyote akisema, ‘Huu ndio mzigo wa
BWANA,’ nitamwadhibu huyo na nyumba
yake. 35 [f]Hivyo mnaambiana kila mmoja
na mwenzake, au kwa mtu wa nyumba
yao: ‘BWANA amejibu nini?’ au ‘BWANA
amesema nini?’ 36 [g]Lakini kamwe msiseme
tena, ‘Nina mzigo wa BWANA,’ kwa sababu
kila neno la mtu binafsi linakuwa mzigo
wake mwenyewe, na hivyo kupotosha
maneno ya Mungu aliye hai, BWANA
Mwenye Nguvu Zote, Mungu wetu. 37 Hivi
ndivyo utakavyoendelea kumuuliza
nabii: ‘BWANA amekujibu nini?’ au ‘Je,
BWANA amesema nini?’ 38 Ingawa unadai,
‘Huu ndio mzigo wa BWANA,’ hili ndilo
BWANA asemalo: Ulitumia maneno, ‘Huu
ndio mzigo wa BWANA,’ hata ingawa
nilikuambia kuwa kamwe usiseme, ‘Huu
ni mzigo wa BWANA.’ 39 [h]Kwa hiyo, hakika
nitakusahau na kukutupa mbali na uso
wangu pamoja na mji niliowapa ninyi na
baba zenu. 40 [i]Nitaleta juu yako fedheha ya
kudumu: yaani aibu ya kudumu ambayo
haitasahaulika.”

*Vikapu Viwili Vya Tini*

24 [j]Baada ya Yekonia[k] mwana wa
Yehoyakimu mfalme wa Yuda, pamoja
na maafisa, mafundi stadi na wahunzi wa
Yuda, kuchukuliwa kutoka Yerusalemu
kwenda Babeli na Nebukadneza mfalme
wa Babeli kwenda uhamishoni huko Babeli,
BWANA akanionyesha vikapu viwili vya tini
vilivyowekwa mbele ya Hekalu la BWANA.
2 [l]Kikapu kimoja kilikuwa na tini nzuri sana,
kama zile za mavuno ya kwanza. Kikapu
cha pili kilikuwa na tini dhaifu sana, mbovu
mno zisizofaa kuliwa.

3 [m]Kisha BWANA akaniuliza, “Je, Yeremia,
unaona nini?”

Nikamjibu, “Ninaona tini zile zilizo nzuri
ni nzuri sana, lakini zilizo dhaifu ni mbovu
mno zisizofaa kuliwa.”

4 Kisha neno la BWANA likanijia:
5 [n]“Hili ndilo BWANA, Mungu wa Israeli,
asemalo: ‘Kama zilivyo hizi tini nzuri,
ndivyo ninavyowaona kuwa bora watu
wa uhamisho kutoka Yuda, niliowaondoa
kutoka mahali hapa kwenda katika nchi
ya Wakaldayo. 6 [o]Macho yangu yatakuwa
juu yao kwa ajili ya kuwapatia mema,
nami nitawarudisha tena katika nchi
hii. Nitawajenga wala sitawabomoa,

---

[a]**23:29** Za 39:3; 1Kor 3:13; 1Pet 4:10; Yer 5:14; Ebr 4:12
[b]**23:30** Za 34:16; Kum 18:20; Yer 21:13; 14:15
[c]**23:32** Mao 2:14; Sef 3:4; Yer 7:8; 50:6; Ay 13:4; Eze 13:3; 22:28; Yer 14:14
[d]**23:33** 2Fal 21:14; Yer 17:15; Mal 1:1
[e]**23:34** Mao 2:14; Zek 13:3
[f]**23:35** Yer 33:3; 42:4
[g]**23:36** Gal 1:7-8; 2Pet 3:16; Yos 3:10
[h]**23:39** Yer 7:15
[i]**23:40** Yer 20:11; Eze 5:14-15
[j]**24:1** 2Fal 24:16; 2Nya 36:9; Kut 23:19; Kum 26:2; Amo 8:1-2
[k]1 Yekonia au Konia ni jina jingine la Yehoyakini.
[l]**24:2** Wim 2:13; Isa 5:4
[m]**24:3** Yer 1:11; Amo 8:1-2
[n]**24:5** Yer 29:4, 20
[o]**24:6** Kum 30:3; Eze 11:17; Yer 42:10; 30:9; Amo 9:14-15

nitawapanda wala sitawang’oa, 7 [a]nitawapa
moyo wa kunifahamu mimi, kwamba mimi
ndimi Bwana. Watakuwa watu wangu,
nami nitakuwa Mungu wao, kwa maana
watanirudia kwa moyo wao wote.
8 [b]“ ‘Lakini kama zilivyo zile tini dhaifu,
ambazo ni mbovu mno zisizofaa kuliwa,’
asema Bwana, ‘ndivyo nitakavyomtendea
Sedekia mfalme wa Yuda, maafisa wake na
mabaki wengine kutoka Yerusalemu, wawe
wamebaki katika nchi hii, au wanaishi
Misri. 9 [c]Nitawafanya kuwa chukizo kabisa
na kitu cha kulaumiwa katika mataifa
yote ya dunia, watakuwa aibu na kitu
cha kudharauliwa, chombo cha dhihaka
na kulaaniwa, popote nitakapowafukuzia.
10 [d]Nitautuma upanga, njaa na tauni dhidi
yao hadi wawe wameangamia kutoka nchi
niliyowapa wao na baba zao.’ ”

*Miaka Sabini Ya Kuwa Mateka*

25 [e]Neno likamjia Yeremia kuhusu watu
wote wa Yuda, katika mwaka wa nne
wa utawala wa Yehoyakimu mwana wa
Yosia mfalme wa Yuda, ambao ulikuwa
mwaka wa kwanza wa utawala wa
Nebukadneza mfalme wa Babeli. 2 [f]Hivyo
nabii Yeremia akawaambia watu wote wa
Yuda na wale wote waishio Yerusalemu:
3 [g]Kwa miaka ishirini na mitatu, kuanzia
mwaka wa kumi na tatu wa utawala wa
Yosia mwana wa Amoni mfalme wa Yuda,
hadi siku hii ya leo, neno la Bwana
limekuwa likinijia, nami nimesema nanyi
mara kwa mara, lakini hamkusikiliza.
4 [h]Ingawa Bwana amewatuma watumishi
wake wote hao manabii kwenu mara kwa
mara, hamkusikiliza wala hamkujali.
5 Walisema, “Geukeni sasa, kila mmoja
wenu kutoka njia yake mbaya na matendo
yake maovu, ndipo mtaweza kukaa katika
nchi ambayo Bwana aliwapa ninyi na baba
zenu milele. 6 [i]Msiifuate miungu mingine
ili kuitumikia na kuiabudu. Msinikasirishe
kwa vitu ambavyo mmevitengeneza kwa
mikono yenu.”
7 [j]“Lakini ninyi hamkunisikiliza
mimi, tena mkanikasirisha kwa vitu
mlivyovitengeneza kwa mikono yenu, nanyi
mmejiletea madhara juu yenu wenyewe,”
asema Bwana.
8 Kwa hiyo Bwana Mwenye Nguvu Zote
asema hivi: “Kwa sababu hamkuyasikiliza
maneno yangu, 9 [k]nitayaita mataifa
yote ya kaskazini na mtumishi wangu
Nebukadneza mfalme wa Babeli,” asema
Bwana. “Nitawaleta waishambulie nchi hii
na wakazi wake wote, na dhidi ya mataifa
yote yanayowazunguka. Nitawaangamiza
kabisa na kuwafanya kitu cha kuchukiwa
na kudharauliwa, na kuwa magofu daima.
10 [l]Nitawaondolea sauti ya shangwe na
furaha, sauti ya bibi na bwana arusi, sauti
ya mawe ya kusagia, na mwanga wa taa.
11 [m]Nchi hii yote itakuwa ukiwa na isiyofaa
kitu, nayo mataifa haya yatamtumikia
mfalme wa Babeli kwa miaka sabini.”
12 [n]“Lakini miaka sabini itakapotimia,
nitamwadhibu mfalme wa Babeli na taifa
lake na nchi ya Wakaldayo kwa ajili ya
hatia yao,” asema Bwana. “Nitaifanya
kuwa ukiwa milele. 13 [o]Nitaleta juu ya nchi
hiyo mambo yote niliyosema dhidi yake,
yote yaliyoandikwa katika kitabu hiki,
na kutolewa unabii na Yeremia dhidi ya
mataifa yote. 14 [p]Wao wenyewe watakuwa

[a]**24:7** Law 26:12; Ebr 8:10; Yer 32:40; 2Nya 6:37; Eze 11:19; Isa 11:9; 51:18; Zek 2:11
[b]**24:8** Yer 29:17; 39:6-9; 44:26; 46:14; 32:4-5; 44:30
[c]**24:9** Yer 25:18; 34:17; Kum 28:25; 2Fal 22:19; Yer 29:18; Dan 9:7; Yer 15:4
[d]**24:10** Isa 51:19; Ufu 6:8; Yer 27:8; 9:16; 15:2; Kum 28:21
[e]**25:1** 2Fal 24:2; Yer 46:2
[f]**25:2** Yer 18:11
[g]**25:3** 1Nya 3:14; Yer 11:7; 26:5; 7:26; Isa 65:12
[h]**25:4** Yer 6:17; 29:19; 7:25-26
[i]**25:6** Kut 20:3; Kum 8:19
[j]**25:7** Kum 32:21; 2Fal 17:20; Yer 7:19
[k]**25:9** Isa 13:3-5; 14:31; 41:2; 2Nya 29:8; Yer 18:16; Hes 21:2; Eze 12:20
[l]**25:10** Isa 24:8; Eze 26:13; Yer 7:34; Mhu 12:3-4; Mao 5:15; Ufu 18:22-23; 15:5
[m]**25:11** Law 26:31-32; Yer 12:11-12; 28:14; 4:26-27; 2Nya 36:21
[n]**25:12** Yer 27:7; 29:10; Isa 13:19-22; 14:22-23; Mwa 10:10; Za 137:8
[o]**25:13** Isa 30:8
[p]**25:14** Isa 14:6; Yer 50:19; 51:27-28; Ay 21:19; Yer 27:7

watumwa wa mataifa mengi na wafalme
wakuu. Nitawalipizia sawasawa na matendo
yao na kazi ya mikono yao.”

*Kikombe Cha Ghadhabu Ya Mungu*

15 [a]Hili ndilo BWANA, Mungu wa Israeli,
aliloniambia: “Chukua kutoka mkononi
mwangu kikombe hiki kilichojaa divai
ya ghadhabu yangu, na kuyanywesha
mataifa yote ambayo ninakutuma kwao.
16 [b]Watakapoinywa, watapepesuka na
kukasirika sana kwa sababu ya upanga
nitakaoupeleka katikati yao.”
17 [c]Hivyo nikakichukua kikombe kutoka
mkononi mwa BWANA, na kuyafanya
mataifa yote aliyonituma kwao kukinywa:
18 [d]Yaani Yerusalemu na miji ya Yuda,
wafalme wake na maafisa wake, kuwafanya
magofu na kuwa kitu cha kuchukiza, cha
dhihaka na laana, kama walivyo leo; 19 [e]pia
Farao mfalme wa Misri, watumishi wake,
maafisa wake na watu wake wote, 20 [f]pia
wageni wote walioko huko; wafalme wote
wa nchi ya Usi; wafalme wote wa Wafilisti
(wale wa Ashkeloni, Gaza, Ekroni na watu
walioachwa huko Ashdodi); 21 [g]Edomu,
Moabu na Amoni; 22 [h]wafalme wote wa
Tiro na Sidoni; wafalme wa nchi za pwani
ng’ambo ya bahari; 23 [i]Dedani, Tema, Buzi
na wote walio maeneo ya mbali; 24 [j]wafalme
wote wa Arabuni na wafalme wote wa
watu wageni wanaoishi katika jangwa;
25 [k]wafalme wote wa Zimri, Elamu na
Umedi; 26 [l]na wafalme wote wa pande za
kaskazini, wa karibu na wa mbali, mmoja
baada ya mwingine; yaani falme zote juu ya
uso wa dunia. Baada ya hao wote, mfalme
wa Sheshaki[m] atakunywa pia.
27 [n]“Kisha uwaambie, ‘Hili ndilo BWANA
Mwenye Nguvu Zote, Mungu wa Israeli,
asemalo: Kunyweni, mlewe na mtapike;
angukeni, wala msiinuke tena kwa sababu
ya upanga nitakaotuma miongoni mwenu.’
28 Lakini kama wakikataa kupokea kikombe
kutoka mikononi mwako na kunywa,
waambie, ‘Hili ndilo asemalo BWANA
Mwenye Nguvu Zote: Ni lazima mnywe!
29 [o]Tazama, nimeanza kuleta maafa juu ya
mji ulio na Jina langu, na je, kweli ninyi
mtaepuka kuadhibiwa? Hamwezi kuepuka
kuadhibiwa, kwa maana nitaleta vita juu
ya wote waishio duniani, asema BWANA
Mwenye Nguvu Zote.’
30 [p]“Basi sasa toa unabii kwa maneno
haya yote dhidi yao, uwaambie:

“ ‘BWANA atanguruma kutoka juu;
atatoa sauti ya ngurumo
kutoka makao yake matakatifu
na kunguruma kwa nguvu sana
dhidi ya nchi yake.
Atapiga kelele kama wao
wakanyagao zabibu,
atapiga kelele dhidi ya wote
waishio duniani.
31 [q]Ghasia zitasikika hadi miisho ya
dunia,
kwa maana BWANA ataleta
mashtaka dhidi ya mataifa;
ataleta hukumu juu ya wanadamu
wote
na kuwaua waovu wote,’ ”
asema BWANA.

[a]**25:15** Za 75:8; Ufu 14:10; Ay 21:20; Isa 51:17; Yer 49:12; Mao 4:21; Eze 23:31
[b]**25:16** Za 60:3; Nah 3:11; Yer 51:7
[c]**25:17** Yer 1:10; 27:3
[d]**25:18** Yer 24; 9; Mwa 19:13; Yer 44:22; 13:13; Ay 12:19; 2Nya 29:8
[e]**25:19** 2Fal 18:21; Isa 20:3; Eze 29:2; Yer 44:30
[f]**25:20** Mwa 10:23; Yer 47:5; Amo 1:7-8; Yos 13:3; Sef 2:4-7; Mwa 10:19
[g]**25:21** Mwa 19:38; Yer 27:3; Mwa 25:30; Kum 23:6
[h]**25:22** Mwa 10:15; Yer 47:4; Dan 11:18; Isa 11:11; Yos 19:29; Isa 48:20; Yer 31:10
[i]**25:23** Mwa 25:3, 15; 22:21; Yer 9:26; 49:32
[j]**25:24** 2Nya 9:14; Yer 50:37
[k]**25:25** Mwa 25:2; 10:22; Isa 21:2
[l]**25:26** Yer 51:41; 50:3-9; Isa 23:17
[m]26 Sheshaki ni Babeli kwa fumbo.
[n]**25:27** Isa 29:9; Nah 3:18; Hab 2:16; Eze 14:17; 21:4; Yer 51:57; Eze 23:32-34
[o]**25:29** Mit 11:31; 1Pet 4:17; Isa 10:12; 2Sam 5:7; Eze 38:21; Yer 13:12-14; Isa 34:2
[p]**25:30** Isa 42:13; 16:10; Yoe 3:16; Za 46:6; Isa 63:3; Ufu 14:19-20
[q]**25:31** Hos 4:1; Mik 6:2; Yer 23:19; 1Sam 12:7; Yer 2:9, 35; Eze 36:5; Yer 15:9

32 [a]Hili ndilo Bwana Mwenye Nguvu Zote asemalo:

“Tazama! Maafa yanaenea
kutoka taifa moja hadi jingine;
tufani kubwa inainuka
kutoka miisho ya dunia.”

33 [b]Wakati huo, hao waliouawa na Bwana watatapakaa kila mahali, kuanzia mwisho mmoja wa dunia hadi mwisho mwingine. Hawataombolezewa wala kukusanywa au kuzikwa, lakini watakuwa kama mavi yaliyoenea juu ya ardhi.

34 [c]Lieni na kuomboleza, enyi
wachungaji,
mgaagae mavumbini,
ninyi viongozi wa kundi.
Kwa maana wakati wenu wa
kuchinjwa umewadia;
mtaanguka na kuvunjavunjwa
kama vyombo vizuri vya udongo.
35 [d]Wachungaji hawatakuwa na mahali
pa kukimbilia,
viongozi wa kundi hawatapata
mahali pa kutorokea.
36 [e]Sikia kilio cha wachungaji,
maombolezo ya viongozi wa
kundi,
kwa maana Bwana anayaharibu
malisho yao.
37 Makao yao ya amani yataharibiwa
kwa sababu ya hasira kali ya
Bwana.
38 [f]Kama simba ataacha pango lake,
nchi yao itakuwa ukiwa
kwa sababu ya upanga wa
mdhalimu,
na kwa sababu ya hasira kali ya
Bwana Mungu.

[a]**25:32** Isa 34:2; Yer 23:19; Isa 30:25; Kum 28:49
[b]**25:33** Eze 39:17-20; Isa 66:16; Yer 16:4; Isa 34:2-8; Yer 8:2; Za 79:3
[c]**25:34** Yer 6:26; Za 44:22; Zek 11:4-7; Yer 2:8; Zek 10:3; Isa 34:6; Yer 50:27
[d]**25:35** Ay 11:20
[e]**25:36** Yer 6:26; 23:1; Zek 11:3
[f]**25:38** Ay 10:16; Yer 4:7; 44:22; 4:26; 46:16; 50:16; Kut 15:7

*Yeremia Atishiwa Kuuawa*

26 [g]Mwanzoni mwa utawala wa
Yehoyakimu mwana wa Yosia
mfalme wa Yuda, neno hili lilikuja
kutoka kwa Bwana: 2 [h]“Hili ndilo Bwana
asemalo: Simama katika ua wa nyumba
ya Bwana na useme na watu wote wa
miji ya Yuda wanaokuja kuabudu katika
nyumba ya Bwana. Waambie kila kitu
nitakachokuamuru, usipunguze neno.
3 [i]Huenda watasikiliza, na kila mmoja
akageuka kutoka njia yake mbaya. Kisha
nitawahurumia na kuacha kuwaletea maafa
niliyokuwa ninapanga kwa sababu ya
maovu waliyofanya. 4 [j]Waambie, ‘Hili ndilo
asemalo Bwana: Ikiwa hamtanisikiliza na
kuifuata sheria yangu ambayo nimeiweka
mbele yenu, 5 [k]nanyi ikiwa hamtayasikiliza
maneno ya watumishi wangu manabii,
ambao nimewatuma kwenu tena na tena
(ijapokuwa hamkuwasikiliza), 6 [l]ndipo
nitaifanya nyumba hii kama Shilo na mji
huu kuwa kitu cha kulaaniwa na mataifa
yote ya dunia.’ ”
7 Makuhani, manabii na watu wote
wakamsikia Yeremia akiyasema maneno
haya ndani ya nyumba ya Bwana. 8 [m]Lakini
mara tu Yeremia alipomaliza kuwaambia
watu kila kitu Bwana alichomwamuru
kukisema, basi makuhani, manabii na
watu wote walimkamata wakisema, “Ni
lazima ufe! 9 [n]Kwa nini unatoa unabii
katika jina la Bwana kwamba nyumba hii
itakuwa kama Shilo na mji huu utakuwa
ukiwa na kuachwa tupu?” Nao watu wote
wakamkusanyikia na kumzunguka Yeremia
ndani ya nyumba ya Bwana.
10 [o]Maafisa wa Yuda waliposikia kuhusu

[g]**26:1** 2Fal 23:36
[h]**26:2** Yer 19:14; Kut 23:14; Mdo 20:27; Kum 12:5; Yer 17:19; Mt 28:20; Kum 4:2
[i]**26:3** Kum 30:2; Isa 55:7; Yer 18:8; 2Nya 33:12-13; Yer 35:15; 36:7
[j]**26:4** Law 26:14; Yer 25:3; 1Fal 9:6; Yer 11:8
[k]**26:5** Mit 1:24; Isa 65:12; Yer 7:13; 25:4; 44:5
[l]**26:6** Yos 18:1; Amu 18:31; Kum 28:25; 2Fal 22:19
[m]**26:8** Mdo 6:12; 21:27; Law 24:15-16; Neh 9:26; Yer 11:21
[n]**26:9** Law 26:32; Yer 9:11; Mdo 21:32
[o]**26:10** Yer 34:19; Eze 22:27; Mwa 23:10

mambo haya, wakapanda kutoka jumba
la kifalme, wakaenda katika nyumba ya
BWANA na kushika nafasi zao kwenye
ingilio la Lango Jipya la nyumba ya
BWANA. 11 [a]Kisha makuhani na manabii
wakawaambia maafisa pamoja na watu
wote, “Mtu huyu anastahili ahukumiwe kifo
kwa sababu ametoa unabii mbaya dhidi
ya mji huu. Mmesikia kwa masikio yenu
wenyewe!”
12 [b]Kisha Yeremia akawaambia maafisa
wote na watu wote: “BWANA amenituma
kutoa unabii dhidi ya nyumba hii na mji
huu mambo yote mliyoyasikia. 13 [c]Sasa
tengenezeni njia zenu na matendo yenu,
na kumtii BWANA Mungu wenu. Ndipo
BWANA atawahurumia na kuacha kuleta
maafa aliyokuwa ameyatamka dhidi
yenu. 14 [d]Lakini kwa habari yangu mimi,
niko mikononi mwenu, nifanyieni lolote
mnaloona kuwa ni jema na la haki. 15 [e]Hata
hivyo, jueni kwa hakika, ikiwa mtaniua,
mtakuwa mmejipatia dhambi kwa damu
isiyo na hatia juu yenu wenyewe, na juu ya
mji huu na wote wanaoishi ndani yake, kwa
maana ni kweli BWANA amenituma kwenu
ili niseme maneno haya yote masikioni
mwenu.”
16 [f]Kisha maafisa na watu wote
wakawaambia makuhani na manabii,
“Mtu huyu asihukumiwe kifo! Amesema
nasi katika jina la BWANA, Mungu wetu.”
17 Baadhi ya wazee wa nchi wakasogea
mbele, wakaliambia kusanyiko lote la
watu, 18 [g]“Mika Mmoreshethi alitoa unabii
katika siku za Hezekia mfalme wa Yuda.
Akawaambia watu wote wa Yuda, ‘Hili
ndilo asemalo BWANA Mwenye Nguvu Zote:

“ ‘Sayuni italimwa kama shamba,
Yerusalemu itakuwa lundo la
kokoto,
na kilima cha Hekalu kitakuwa
kichuguu
kilichofunikwa na vichaka.’

19 [h]Je, Hezekia mfalme wa Yuda au mtu
mwingine yeyote katika Yuda alimhukumu
Mika kufa? Je, Hezekia hakumcha BWANA
na kuhitaji msaada wake? Je, BWANA
hakuwahurumia na akaacha kuleta
maafa aliyokuwa ametamka dhidi yao?
Tunakaribia sana kujiletea maangamizo
ya kutisha sisi wenyewe!”
20 [i](Wakati huu, Uria mwana wa Shemaya
kutoka mji wa Kiriath-Yearimu alikuwa
mtu mwingine aliyetoa unabii kwa jina
la BWANA. Alitoa unabii juu ya mambo
yaliyofanana na haya dhidi ya mji huu
na nchi hii kama alivyofanya Yeremia.
21 [j]Mfalme Yehoyakimu na wakuu wake
wote na maafisa waliposikia maneno yake,
mfalme alitafuta kumuua. Lakini Uria
alipata habari, na kwa kuogopa akakimbilia
Misri. 22 [k]Hata hivyo, Mfalme Yehoyakimu
alimtuma Elnathani mwana wa Akbori huko
Misri, pamoja na watu wengine ili kwenda
kumkamata Uria. 23 [l]Wakamrudisha Uria
kutoka Misri na kumpeleka kwa Mfalme
Yehoyakimu, ambaye alimuua kwa upanga,
na mwili wake kutupwa kwenye eneo la
makaburi ya watu wasio na cheo.)
24 [m]Zaidi ya hayo, Ahikamu mwana wa
Shafani akamuunga mkono Yeremia, kwa
hiyo hakutiwa tena mikononi mwa watu
ili auawe.

### *Yuda Kumtumikia Nebukadneza*

27 [n]Mwanzoni mwa utawala wa
Yehoyakimu mwana wa Yosia mfalme
wa Yuda, neno hili lilimjia Yeremia

[a]**26:11** Yer 38:4; Kum 18:20; Mdo 6:11; Kum 18:20
[b]**26:12** Yer 1:18; Isa 6:8; Mdo 5:29; Amo 7:15; Mdo 4:18-20
[c]**26:13** Yoe 2:12; Yer 7:5; 35:15; 11:4; 18:8
[d]**26:14** Yos 9:15; Yer 38:5
[e]**26:15** Kum 19:10; Yer 1:17
[f]**26:16** Mdo 23:9; 5:34-39; 23:29
[g]**26:18** Isa 2:3; 2Fal 25:9; Neh 4:2; Mik 1:4; Zek 8:3; Yer 17:3; 9:11
[h]**26:19** 1Nya 3:13; Kut 32:14; Isa 37:14-20; 2Sam 24:16; Hab 2:10; 2Nya 32:24-26
[i]**26:20** Yos 9:17
[j]**26:21** Mwa 31:21; Mt 10:23; 1Fal 19:2-3; Yer 2:30; Mt 23:37
[k]**26:22** Yer 36:12, 25; Mit 29:12
[l]**26:23** 2Fal 23:6; Ebr 11:37
[m]**26:24** 2Fal 22:12; Yer 39:14
[n]**27:1** 2Nya 36:11; Yer 28:1

kutoka kwa BWANA: 2 [a]Hili ndilo BWANA
aliloniambia: “Tengeneza nira, ujivike
shingoni mwako, uifunge kwa kamba za
ngozi. 3 [b]Kisha utume ujumbe kwa wafalme
wa Edomu, Moabu, Amoni, Tiro na Sidoni
kupitia wajumbe ambao wamekuja
Yerusalemu kwa Sedekia mfalme wa Yuda.
4 Wape ujumbe kwa ajili ya mabwana zao
na uwaambie: Hili ndilo asemalo BWANA
Mwenye Nguvu Zote, Mungu wa Israeli:
‘Waambieni hivi mabwana zenu: 5 [c]Kwa
uwezo wangu mkuu na kwa mkono wangu
ulionyooshwa nimeumba dunia na watu
wake na wanyama walioko ndani yake,
nami humpa yeyote inipendezavyo. 6 [d]Sasa
nitazitia nchi zenu zote mkononi mwa
mtumishi wangu Nebukadneza mfalme
wa Babeli, na nitawafanya hata wanyama
wa mwituni wamtumikie. 7 [e]Mataifa yote
yatamtumikia yeye, pamoja na mwanawe
na mwana wa mwanawe, hadi wakati wa
nchi yake utakapowadia, kisha mataifa
mengi na wafalme wenye nguvu nyingi
watamshinda.

8 “ ‘ “Lakini kama kukiwa na taifa
lolote au ufalme ambao hautamtumikia
Nebukadneza mfalme wa Babeli, ama
kuinamisha shingo yake chini ya nira
yake, nitaliadhibu taifa hilo kwa upanga,
njaa na tauni, asema BWANA, mpaka
nitakapoliangamiza taifa hilo kwa mkono
wake. 9 [f]Kwa hiyo msiwasikilize manabii
wenu, waaguzi wenu, waota ndoto wenu,
watabiri na wachawi wanaowaambia
ninyi: Hamtamtumikia mfalme wa Babeli.
10 [g]Wanawatabiria uongo ambao utawafanya
ninyi mhamishwe mbali kutoka nchi yenu.
Nitawafukuzia mbali, nanyi mtaangamia.
11 [h]Lakini ikiwa taifa lolote litainama na
kuweka shingo lake katika nira ya mfalme
wa Babeli na kumtumikia, nitaliacha taifa
hilo katika nchi yake yenyewe ili wailime
na kuishi humo, asema BWANA.” ’ ”

12 [i]Nilitoa ujumbe huo huo kwa Sedekia
mfalme wa Yuda. Nilisema, “Ingiza
shingo yako katika nira ya mfalme wa
Babeli, umtumikie yeye na watu wake,
nawe utaishi. 13 [j]Kwa nini wewe na watu
wako mfe kwa upanga, njaa na tauni,
ambazo BWANA ameonya juu ya taifa
lolote ambalo halitamtumikia mfalme wa
Babeli? 14 [k]Msiyasikilize maneno ya manabii
wanaowaambia kwamba, ‘Hamtamtumikia
mfalme wa Babeli,’ kwa sababu
wanawatabiria uongo. 15 [l]“Sikuwatuma
hao,’ asema BWANA. ‘Wanatabiri uongo
kwa jina langu. Kwa hiyo, nitawafukuzia
mbali, nanyi mtaangamia, ninyi pamoja na
manabii wanaowatabiria.’ ”

16 [m]Kisha nikawaambia makuhani na
watu hawa wote, “Hili ndilo asemalo
BWANA: Msiwasikilize manabii
wanaosema, ‘Hivi karibuni sana vyombo
vya nyumba ya BWANA vitarudishwa
kutoka Babeli.’ Wanawatabiria ninyi
uongo. 17 [n]Msiwasikilize. Mtumikieni
mfalme wa Babeli, nanyi mtaishi. Kwa
nini mji huu uwe magofu? 18 [o]Kama wao
ni manabii na wanalo neno la BWANA,
basi na wamsihi BWANA Mwenye Nguvu
Zote ili vyombo vilivyobaki katika nyumba
ya BWANA na katika jumba la kifalme la
mfalme wa Yuda na katika Yerusalemu
visipelekwe Babeli. 19 [p]Kwa maana hili
ndilo asemalo BWANA Mwenye Nguvu
Zote kuhusu zile nguzo, ile Bahari, vile
vishikizo viwezavyo kuhamishika, vinara

[a]**27:2** Law 26:13; Yer 28:10-13; 1Fal 22:11
[b]**27:3** Yer 25:17, 21; Mwa 10:15; Yer 25:21-22
[c]**27:5** Kum 9:29; Za 115:16; Dan 4:17; Mwa 1:25
[d]**27:6** Yer 25:9; 21:7; Eze 29:18-20; Dan 2:37-38; Yer 28:14
[e]**27:7** Dan 5:18, 28; Yer 25:12; 2Nya 36:20; Yer 51:47; 25:14
[f]**27:9** Kum 18:11; Efe 5:6; Mit 19:27; Eze 13:1-23; Mwa 30:27; Isa 44:25; Kut 7:11; Yer 6:14
[g]**27:10** Yer 23:25; Mk 13:5; 2Fal 23:27
[h]**27:11** Yer 21:9; Kum 6:2
[i]**27:12** Yer 17:4; 21:9
[j]**27:13** Eze 18:31; Mit 8:36; Yer 14:12
[k]**27:14** Yer 14:14; Mt 7:15; Yer 23:16-21
[l]**27:15** Yer 23:21-29; 9; 44:16; 6:15; Mt 15:12-14
[m]**27:16** 1Fal 7:48-50; Yer 28:3; Dan 1:2; 2Fal 24:13
[n]**27:17** Yer 23:16; 42:11
[o]**27:18** Hes 21:7; 1Sam 7:8; Ay 42; 8; Yak 5:16
[p]**27:19** 1Fal 7:23-26; 2Fal 25:13; Yer 52:17-23

na vyombo vingine vilivyoachwa katika mji
huu, 20 [a]ambavyo Nebukadneza mfalme wa
Babeli hakuvichukua wakati alipomchukua
Yekonia[b] mwana wa Yehoyakimu mfalme
wa Yuda kwenda uhamishoni huko Babeli
kutoka Yerusalemu, pamoja na wakuu
wote wa Yuda na Yerusalemu. 21 Naam,
hili ndilo BWANA Mwenye Nguvu Zote,
Mungu wa Israeli, asemalo kuhusu vitu
ambavyo vimebaki ndani ya nyumba ya
BWANA, na ndani ya jumba la kifalme la
mfalme wa Yuda, na katika Yerusalemu:
22 [c]'Vitachukuliwa kupelekwa Babeli, nako
huko vitabaki mpaka siku nitakayovijilia,'
asema BWANA. 'Kisha nitavirudisha na
kuvirejesha mahali hapa.' "

*Hanania Nabii Wa Uongo*

28 [d]Katika mwezi wa tano wa mwaka ule
ule, yaani mwaka wa nne, mwanzoni
mwa utawala wa Sedekia mfalme wa Yuda,
nabii Hanania mwana wa Azuri, ambaye
alitoka Gibeoni, akaniambia katika nyumba
ya BWANA mbele ya makuhani na watu
wote: 2 [e]"Hili ndilo BWANA Mwenye Nguvu
Zote, Mungu wa Israeli asemalo: 'Nitaivunja
nira ya mfalme wa Babeli. 3 [f]Katika muda
wa miaka miwili nitavirudisha mahali hapa
vyombo vyote vya nyumba ya BWANA
ambavyo Nebukadneza mfalme wa Babeli
aliviondoa kutoka hapa na kuvipeleka
Babeli. 4 [g]Pia nitamrudisha mahali hapa
Yekonia[h] mwana wa Yehoyakimu mfalme
wa Yuda, pamoja na wote waliohamishwa
kutoka Yuda ambao walikwenda Babeli,'
asema BWANA, 'kwa kuwa nitaivunja nira
ya mfalme wa Babeli.' "
5 Ndipo nabii Yeremia akamjibu nabii
Hanania mbele ya makuhani na watu wote
waliokuwa wamesimama ndani ya nyumba
ya BWANA. 6 [i]Akasema, "Amen! BWANA na
afanye hivyo! BWANA na ayatimize maneno
uliyotoa unabii kwa kuvirudisha mahali
hapa kutoka Babeli vyombo vya nyumba
ya BWANA pamoja na wote waliohamishwa.
7 Hata hivyo, nisikilize nikuambie yale
nitakayoyasema masikioni mwako na
masikioni mwa watu hawa wote: 8 [j]Tangu
mwanzo, manabii waliokutangulia wewe na
mimi walitabiri vita, maafa na tauni dhidi
ya nchi nyingi na falme kubwa. 9 [k]Lakini
nabii atakayetabiri amani atatambuliwa
kuwa kweli ametumwa na BWANA ikiwa
unabii wake utatimia."
10 [l]Kisha nabii Hanania akaiondoa
nira iliyokuwa shingoni mwa Yeremia
na kuivunja, 11 [m]naye akasema mbele ya
watu wote, "Hili ndilo asemalo BWANA:
'Vivi hivi ndivyo nitakavyoivunja nira ya
Nebukadneza mfalme wa Babeli kutoka
kwenye shingo za mataifa katika muda huu
wa miaka miwili.' " Alipofanya hivi, nabii
Yeremia akaondoka zake.
12 Kitambo kidogo baada ya nabii
Hanania kuivunja nira kutoka shingo ya
nabii Yeremia, neno la BWANA likamjia
Yeremia: 13 "Nenda ukamwambie Hanania,
'Hili ndilo asemalo BWANA: Umevunja nira
ya mti, lakini badala yake utapata nira
ya chuma. 14 [n]Hili ndilo asemalo BWANA
Mwenye Nguvu Zote, Mungu wa Israeli:
Nitaweka nira ya chuma kwenye shingo za
mataifa haya yote ili kufanya yamtumikie
Nebukadneza mfalme wa Babeli, nao
watamtumikia. Nitampa kutawala hata
wanyama wa mwituni.' "
15 [o]Kisha nabii Yeremia akamwambia

[a]**27:20** Kum 28:36; 2Nya 36:10; Yer 22:24; Mt 1:11
[b]20 Yekonia au Konia ni jina jingine la Yehoyakini.
[c]**27:22** 2Fal 20:17; 2Nya 25:13; 36:21; Yer 24:6; Ezr 7:19
[d]**28:1** Yer 27:1-3; Yos 9:3; 2Nya 36:11
[e]**28:2** Yer 27:12
[f]**28:3** 2Fal 24:13; Yer 27:16-22
[g]**28:4** Yer 22:24-27; 2Fal 25:30; Hos 7:3
[h]4 Yekonia au Konia ni jina jingine la Yehoyakini.
[i]**28:6** 1Nya 16:36; Za 72:19; 1Kor 14:16; Ufu 1:18; Zek 6:10
[j]**28:8** Isa 5:5-7; Nah 1:14
[k]**28:9** Kum 18:22; Eze 33:33; Isa 8:20
[l]**28:10** Law 26:13; Yer 27:2; Za 10:13; 1Fal 22:11
[m]**28:11** Yer 14:14; 27:10; Mit 26:4
[n]**28:14** Kum 28:48; Yer 15:12; 25:11; 27:4-7; Dan 8:15; Yer 39:1
[o]**28:15** Yer 29:31; Mao 2:14; Eze 13:6; Yer 7:4; 20:6; 29:21

nabii Hanania, "Sikiliza Hanania! BWANA
hajakutuma, lakini wewe umelishawishi
taifa hili kuamini uongo. 16 [a]Kwa hiyo,
hili ndilo asemalo BWANA: 'Hivi karibuni
nitakuondoa kutoka juu ya uso wa
dunia. Mwaka huu utakufa, kwa sababu
umetangaza uasi dhidi ya BWANA.' "
17 [b]Katika mwezi wa saba wa mwaka ule
ule, nabii Hanania akafa.

### *Barua Kwa Watu Wa Uhamisho*

29 [c][d]Haya ndiyo maneno ya ile barua
ambayo nabii Yeremia aliituma kutoka
Yerusalemu kwenda kwa wazee waliobaki
miongoni mwa wale waliohamishwa, na
kwa makuhani, manabii na watu wengine
wote ambao Nebukadneza alikuwa
amewachukua kwenda uhamishoni Babeli
kutoka Yerusalemu. 2 [e](Hii ilikuwa ni baada
ya Mfalme Yekonia[f] na malkia mamaye,
maafisa wa mahakama, viongozi wa Yuda
na wa Yerusalemu, mafundi na wahunzi
kwenda uhamishoni kutoka Yerusalemu.)
3 Barua ilikabidhiwa kwa Elasa mwana wa
Shafani, na kwa Gemaria mwana wa Hilkia,
ambao Sedekia mfalme wa Yuda aliwatuma
kwa Mfalme Nebukadneza huko Babeli.
Barua yenyewe ilisema:

4 [g]Hili ndilo BWANA Mwenye Nguvu
Zote, Mungu wa Israeli, awaambialo
wale wote niliowapeleka kutoka
Yerusalemu kwenda uhamishoni
Babeli: 5 "Jengeni nyumba na mstarehe,
pandeni bustani na mle mazao yake.
6 [h]Oeni wake na mzae wana na binti,
waozeni wana wenu wake, nanyi
watoeni binti zenu waolewe, ili nao pia
wazae wana na binti. Ongezekeni idadi
yenu huko, wala msipungue. 7 [i]Pia
tafuteni amani na mafanikio ya mji
ambamo nimewapeleka uhamishoni.
Mwombeni BWANA kwa ajili ya mji
huo, kwa sababu ukistawi, ninyi pia
mtastawi."

8 [j]Naam, hili ndilo BWANA Mwenye
Nguvu Zote, Mungu wa Israeli,
asemalo: "Msikubali manabii na
wabashiri walioko miongoni mwenu
wawadanganye. Msisikilize ndoto
ambazo mmewatia moyo kuota.
9 [k]Wanawatabiria ninyi uongo kwa jina
langu. Sikuwatuma," asema BWANA.
10 [l]Hili ndilo asemalo BWANA:
"Miaka sabini itakapotimia kwa
ajili ya Babeli, nitakuja kwenu na
kutimiza ahadi yangu ya rehema ya
kuwarudisha mahali hapa. 11 [m]Kwa
maana ninajua mipango niliyo nayo
kwa ajili yenu," asema BWANA, "ni
mipango ya kuwafanikisha na wala si
ya kuwadhuru, ni mipango ya kuwapa
tumaini katika siku zijazo. 12 [n]Kisha
mtaniita, na mtakuja na kuniomba,
nami nitawasikiliza. 13 [o]Mtanitafuta na
kuniona, mtakaponitafuta kwa moyo
wenu wote. 14 Nitaonekana kwenu,"
asema BWANA, "nami nitawarudisha
watu wenu waliotekwa. Nitawakusanya
kutoka mataifa yote na mahali pote
nilipokuwa nimewafukuzia, nami
nitawarudisha mahali ambapo
nilikuwa nimewatoa walipochukuliwa
uhamishoni," asema BWANA.
15 Mnaweza mkasema, "BWANA
ameinua manabii kwa ajili yetu huku
Babeli," 16 lakini hili ndilo asemalo
BWANA kuhusu mfalme aketiaye kiti
cha enzi cha Daudi, na watu wa kwenu

[a]**28:16** Mwa 7:4; Kum 13:5; Yer 29:32; Kum 18:20; Zek 13:3
[b]**28:17** 1Sam 2:9; Ay 21:30; Rum 2:2-3; 2Fal 1:17
[c]**29:1** 2Nya 36:10; Yer 13:17
[d]**29:1** Eze 39:25; Rum 10:20; Sef 3:20; Yer 46:27; Eze 37:21; Kum 30:3; Yer 30:3
[e]**29:2** 2Fal 24:12; Yer 22:24-28; 2Fal 24:8
[f]2 Yekonia au Konia ni jina jingine la Yehoyakini.
[g]**29:4** Yer 24:5
[h]**29:6** Yer 30:19
[i]**29:7** Ebr 6:10; 1Tim 2:1-2; Rum 13:1-5; Es 3:8
[j]**29:8** Yer 37:9; 23:21-27; 1Yn 4:1; Kum 13:1
[k]**29:9** Mao 2:14; Eze 13:6; Yer 27:15; 23:21
[l]**29:10** 2Nya 36:21; Dan 9:2; Yer 16:14; 24:6; 32:42; 1Fal 8:56
[m]**29:11** Za 40:5; Zek 8:15; Isa 55:12
[n]**29:12** Za 145:19; Isa 55:6; Dan 9:3; Hos 2:23; Sef 3:12; Zek 13:9
[o]**29:13** Mt 7:7; Kum 4:29; 2Nya 6:37; Yer 24:7

wote wanaobaki katika mji huu, ndugu
zenu ambao hawakwenda pamoja
nanyi uhamishoni. 17 [a]Naam, hili ndilo
asemalo BWANA Mwenye Nguvu Zote:
"Nitatuma upanga, njaa na tauni dhidi
yao, nami nitawafanya kuwa kama tini
dhaifu zile ambazo ni mbovu sana
zisizofaa kuliwa. 18 [b]Nitawafukuza kwa
upanga, kwa njaa na kwa tauni, nami
nitawafanya kitu cha kuchukiza sana
kwa falme zote za dunia, na kuwa kitu
cha laana na cha kuogofya, cha dharau
na kukemewa, miongoni mwa mataifa
yote nitakakowafukuzia. 19 [c]Kwa kuwa
hawakuyasikiliza maneno yangu,"
asema BWANA, "maneno ambayo
niliwatumia tena na tena kupitia
watumishi wangu manabii. Wala ninyi
watu wa uhamisho hamkusikiliza pia,"
asema BWANA.

20 [d]Kwa hiyo, sikieni neno la
BWANA, enyi nyote mlio uhamishoni,
niliowapeleka Babeli kutoka
Yerusalemu. 21 [e]Hili ndilo BWANA
Mwenye Nguvu Zote, Mungu wa
Israeli, asemalo kuhusu Ahabu mwana
wa Kolaya, na Sedekia mwana wa
Maaseya, wanaowatabiria uongo
kwa jina langu: "Nitawatia mikononi
mwa Nebukadneza mfalme wa Babeli,
naye atawaua mbele ya macho yenu
hasa. 22 [f]Kwa ajili yao, watu wote
wa uhamisho kutoka Yuda walioko
Babeli watatumia laana hii: 'BWANA
na akutendee kama Sedekia na Ahabu,
ambao mfalme wa Babeli aliwachoma
kwa moto.' 23 [g]Kwa kuwa wamefanya
mambo maovu kabisa katika Israeli,
wamezini na wake za majirani zao,
tena kwa Jina langu wamesema
uongo, mambo ambayo sikuwaambia
kuyafanya. Nami nayajua haya, na ni
shahidi wa jambo hilo," asema BWANA.

*Ujumbe Kwa Shemaya*

24 Mwambie Shemaya Mnehelami,
25 [h]"Hili ndilo BWANA Mwenye Nguvu Zote,
Mungu wa Israeli, asemalo: Ulituma barua
kwa jina lako mwenyewe kwa watu wote
wa Yerusalemu, kwa Sefania mwana wa
kuhani Maaseya na kwa makuhani wengine
wote. Ulimwambia Sefania, 26 [i]"BWANA
amekuweka wewe uwe kuhani badala ya
Yehoyada ili uwe msimamizi wa nyumba ya
BWANA. Unapaswa kufunga kwa mikatale
na mnyororo wa shingoni mwendawazimu
yeyote anayejifanya nabii. 27 Kwa nini
basi hukumkemea Yeremia Mwanathothi,
aliyejifanya kama nabii miongoni mwenu?
28 Ametutumia ujumbe huu huku Babeli:
Mtakuwako huko muda mrefu. Kwa
hiyo jengeni nyumba mkakae; pandeni
mashamba na mle mazao yake.' "

29 Kuhani Sefania, hata hivyo, akamsomea
nabii Yeremia ile barua. 30 Ndipo neno
la BWANA likamjia Yeremia kusema:
31 [j]"Tuma ujumbe huu kwa watu wote walio
uhamishoni: 'Hili ndilo BWANA asemalo
kuhusu Shemaya Mnehelami: Kwa sababu
Shemaya amewatabiria ninyi, hata ingawa
sikumtuma, naye amewafanya kuamini
uongo, 32 [k]hili ndilo BWANA asemalo: Hakika
nitamwadhibu Shemaya Mnehelami pamoja
na uzao wake. Hapatakuwa na yeyote
atakayebaki miongoni mwa watu hawa,
wala hataona mema nitakayowatendea
watu wangu, asema BWANA, kwa sababu
ametangaza uasi dhidi yangu.' "

*Kurudishwa Kwa Israeli*

30 Hili ndilo neno lililomjia Yeremia
kutoka kwa BWANA: 2 [l]"Hili ndilo
asemalo BWANA, Mungu wa Israeli: 'Andika
katika kitabu maneno yote niliyonena na

[a]**29:17** Yer 24:8-10; 27:8; Isa 5:4
[b]**29:18** Yer 15:4; Kum 28:25; Yer 42:18; Mao 2:18-19; Hes 5:27; Yer 18:16; Isa 28:22
[c]**29:19** Yer 6:19; 32:33; 25:4; 7:25
[d]**29:20** Yer 24:5; Amo 3:6; Mik 4:10
[e]**29:21** Yer 14:14
[f]**29:22** Dan 3:6; Isa 65:15
[g]**29:23** Yer 23:14; Ebr 4:13; Yer 13:27; Sef 3:4; Mwa 31:48; Yer 7:11
[h]**29:25** 2Fal 25:18; Yer 21:1
[i]**29:26** Kum 13:1-5; 1Sam 10:11; 2Fal 9:11; Yer 20:2; Yn 10:20; Hos 9:7
[j]**29:31** Yer 14:14; 28:15
[k]**29:32** 1Sam 2:30-33; Yer 28:16; Rum 2:8
[l]**30:2** Isa 30:8; Yer 36:2

wewe. 3 [a]Siku zinakuja,' asema BWANA,
'nitakapowaleta watu wangu Israeli na Yuda
kutoka uhamishoni, na kuwarudisha katika
nchi niliyowapa baba zao ili kuimiliki,'
asema BWANA."
4 Haya ndiyo maneno BWANA aliyoyanena
kuhusu Israeli na Yuda: 5 [b]"Hili ndilo
asemalo BWANA:

" 'Vilio vya woga vinasikika:
hofu kuu, wala si amani.
6 [c]Ulizeni na mkaone:
Je, mwanaume aweza kuzaa
watoto?
Kwa nini basi ninaona kila
mwanaume mwenye nguvu
ameweka mikono yake tumboni
kama mwanamke aliye na utungu
wa kuzaa,
kila uso ukigeuka rangi kabisa?
7 [d]Tazama jinsi ile siku itakavyokuwa
ya kutisha!
Hakutakuwa na nyingine mfano
wake.
Utakuwa wakati wa dhiki kwa
Yakobo,
lakini ataokolewa kutoka hiyo.

8 [e]" 'Katika siku ile,' asema BWANA
Mwenye Nguvu Zote,
'nitaivunja nira kutoka shingoni
mwao
na kuvipasua vifungo vyao;
wageni hawatawafanya tena
watumwa.
9 [f]Badala yake, watamtumikia BWANA,
Mungu wao
na Daudi mfalme wao,
nitakayemwinua kwa ajili yao.

10 [g]" 'Hivyo usiogope, ee Yakobo
mtumishi wangu,
usifadhaike, ee Israeli,'
asema BWANA.
'Hakika, nitakuokoa kutoka mbali,
wazao wako kutoka nchi ya
uhamisho wao.
Yakobo atakuwa tena na amani na
usalama,
wala hakuna atakayemtia hofu.
11 [h]Mimi niko pamoja nawe, nami
nitakuokoa,'
asema BWANA.
'Ingawa nitayaangamiza kabisa
mataifa yote
ambamo miongoni mwao
nimewatawanya,
sitawaangamiza ninyi kabisa.
Nitawaadhibu, lakini kwa haki.
Sitawaacha kabisa bila adhabu.'

12 [i]"Hili ndilo asemalo BWANA:

" 'Kidonda chako hakina dawa,
jeraha lako haliponyeki.
13 [j]Hakuna yeyote wa kukutetea shauri
lako,
hakuna dawa ya kidonda chako,
wewe hutapona.
14 [k]Wale walioungana nawe wote
wamekusahau,
hawajali chochote kukuhusu
wewe.
Nimekupiga kama vile adui
angelifanya,
na kukuadhibu kama vile mtu
mkatili angelifanya,
kwa sababu hatia yako ni kubwa
mno
na dhambi zako ni nyingi sana.

---

[a]**30:3** Yer 29:14; 16:15; Amo 9:14; Yer 24:6
[b]**30:5** Yer 6:25
[c]**30:6** Yer 4:31; Isa 29:22
[d]**30:7** Isa 2:12; Amo 5:18; Yoe 2:11; Isa 22:5; Sef 1:15; Yer 23:3
[e]**30:8** Isa 9:4; Yer 25:14; Eze 34:27; Yer 27:7; Za 107:14
[f]**30:9** Isa 55:3-4; 1Sam 13:14; Hos 1:11; 3:5; Yer 33:15; Eze 34:23-24
[g]**30:10** Isa 41:10-13; 43:5; Yer 29:14; Isa 35:9; Yer 17:25; Isa 29:22; Eze 34:25-28
[h]**30:11** Law 26:44; Yer 4:27; 10:24; Hos 11:9; Amo 9:8; Yer 5:18; Isa 29:22; Eze 34:25-28
[i]**30:12** Yer 8:22; 15:18; Ay 6:4; Yer 10:19
[j]**30:13** Nah 3:19; Amu 6:31; Yer 14:19; 8:22; 46:11
[k]**30:14** Yer 22:20; Ay 13:24; 30:21; Yer 25:7; Mao 1:2

15 [a]Kwa nini unalia kwa ajili ya jeraha
lako,
yale maumivu yako
yasiyoponyeka?
Kwa sababu ya uovu wako mkubwa
na dhambi zako nyingi
nimekufanyia mambo haya.

16 [b]" 'Lakini watu wote wakuangamizao
wataangamizwa;
adui zako wote watakwenda
uhamishoni.
Wale wote wakutekao nyara
watatekwa nyara;
wote wakufanyao mateka
nitawafanya mateka.
17 [c]Lakini nitakurudishia afya yako
na kuyaponya majeraha yako,'
asema BWANA,
'kwa sababu umeitwa mwenye
kutupwa,
Sayuni ambaye hakuna yeyote
anayekujali.'

18 [d]"Hili ndilo asemalo BWANA:

" 'Nitarudisha baraka za mahema ya
Yakobo,
na kuhurumia maskani yake.
Mji utajengwa tena juu ya magofu
yake,
nalo jumba la kifalme litasimama
mahali pake halisi.
19 [e]Nyimbo za kushukuru zitatoka kwao
na sauti ya furaha.
Nitaiongeza idadi yao
wala hawatapungua,
nitawapa heshima
na hawatadharauliwa.
20 [f]Watoto wao watakuwa kama
walivyokuwa
siku za zamani,
nayo jumuiya yao itaimarishwa
mbele yangu;
nitawaadhibu wale wote
wawaoneao.
21 [g]Mmoja wao atakuwa kiongozi wao;
mtawala wao atainuka miongoni
mwao.
Nitamleta karibu nami,
naye atanikaribia mimi,
kwa maana ni nani yule
atakayejitolea
kuwa karibu nami?'
asema BWANA.
22 [h]'Kwa hiyo ninyi mtakuwa watu
wangu,
nami nitakuwa Mungu wenu.' "

23 [i]Tazama, tufani ya BWANA
italipuka kwa ghadhabu,
upepo wa kisulisuli uendao kasi
utashuka juu ya vichwa vya
waovu.
24 [j]Hasira kali ya BWANA haitarudi
nyuma
mpaka atakapotimiza makusudi
yote ya moyo wake.
Siku zijazo
mtayaelewa haya.

### *Mahamisho Kurudi Kwa Shangwe*

31 [k]"Wakati huo, nitakuwa Mungu wa
koo zote za Israeli nao watakuwa watu
wangu," asema BWANA.
2 [l]Hili ndilo asemalo BWANA:

"Watu watakaopona upanga
watapata upendeleo jangwani;
nitakuja niwape Israeli pumziko."

[a]**30:15** Yer 10:19; Mit 1:31
[b]**30:16** Kum 23:22; Yoe 3:4-8; Isa 29:8; Yer 10:25; Isa 14:2; Yer 49:2; 50:10
[c]**30:17** Isa 6:12; Yer 33:24; Kut 15:26; Za 142:4
[d]**30:18** Kum 30:3; Yer 32:44; Za 103:13; Eze 39:25; 36:10; Yer 31:23; Hes 24:5
[e]**30:19** Neh 8:12; Mwa 15:5; Isa 51:3, 11; 60:9; Yer 31:4; Isa 35:10; 44:23; Zek 2:4
[f]**30:20** Isa 54:13-14; Zek 8:5; Yer 31:17; Kut 23:22
[g]**30:21** Yer 23:5-6; Hes 16:5; Kum 17:15
[h]**30:22** Isa 19:25; Hos 2:23; Law 26:12
[i]**30:23** Yer 23:19; 25:32
[j]**30:24** Yer 4:8; Mao 1:12; Yer 4:28; 23:19-20
[k]**31:1** Law 26:12; Yer 30:22
[l]**31:2** Hes 14:20; Kut 33:14; Kum 12:9

3 [a]BWANA alitutokea wakati uliopita, akisema:

"Nimekupenda kwa upendo wa milele,
nimekuvuta kwa wema.
4 [b]Nitakujenga tena nawe utajengeka upya,
ewe Bikira Israeli.
Utachukua tena matari yako
na kwenda kucheza na wenye furaha.
5 [c]Utapanda tena shamba la mizabibu
juu ya vilima vya Samaria,
wakulima watapanda
na kufurahia matunda yake.
6 [d]Itakuja siku wakati walinzi watakapowapigia kelele
juu ya vilima vya Efraimu wakisema,
'Njooni, twendeni juu Sayuni,
kwake BWANA Mungu wetu.' "

7 [e]Hili ndilo asemalo BWANA:

"Mwimbieni Yakobo kwa furaha,
mpigieni kelele aliye mkuu wa mataifa.
Zifanyeni sifa zenu zisikike, nanyi mseme,
'Ee BWANA, okoa watu wako,
mabaki ya Israeli.'
8 [f]Tazama, nitawaleta kutoka nchi ya kaskazini
na kuwakusanya kutoka miisho ya dunia.
Miongoni mwao watakuwepo vipofu na viwete,
mama wajawazito na wenye utungu wa kuzaa.
Umati mkubwa wa watu utarudi.
9 [g]Watakuja wakilia;
wataomba wakati ninawarudisha.
Nitawaongoza kando ya vijito vya maji
katika mapito yaliyo tambarare ambapo hawatajikwaa,
kwa sababu mimi ndimi baba wa Israeli,
naye Efraimu ni mzaliwa wangu wa kwanza.

10 [h]"Sikieni neno la BWANA, enyi mataifa,
litangazeni katika nchi za pwani ya mbali:
'Yeye aliyewatawanya Israeli atawakusanya
na atalichunga kundi lake la kondoo kama mchungaji.'
11 [i]Kwa kuwa BWANA atamlipia fidia Yakobo
na kuwakomboa mkononi mwa walio na nguvu kuliko wao.
12 [j]Watakuja na kupiga kelele kwa furaha katika miinuko ya Sayuni;
watashangilia ukarimu wa BWANA:
nafaka, divai mpya na mafuta,
wana-kondoo wachanga
na ndama wa makundi ya ng'ombe nitakaowapa.
Watakuwa kama bustani iliyonyeshewa vizuri,
wala hawatahuzunika tena.

[a]**31:3** Rum 11:28; Kum 4:37; Hos 11:4; Yn 6:44
[b]**31:4** Yer 30:18-19; 2Fal 19:21; Mwa 31:27; Kut 15:20; Yer 30:19
[c]**31:5** Yer 33:13; Oba 1:19; Isa 65:12; Amo 9:14; Kum 20:6; Yer 50:19; Isa 37:30
[d]**31:6** Kum 33:19; Mik 4:2; Isa 52:8; 56:10; Yer 50:4-5
[e]**31:7** Kum 28:13; Isa 61:9; Za 14:7; 28:9; Isa 37:31; 12:6
[f]**31:8** Yer 3:18; Mwa 33:13; Za 106:47; Isa 42:16; Eze 34:16; 34:12-14
[g]**31:9** Ezr 3:12; Za 126:5; Isa 63:13; Za 126:5; Isa 63:13; 40:4; 49:11; Kut 4:22; Hes 20:8
[h]**31:10** Isa 66:19; Kum 30:4; Isa 11:12; 40:11; Eze 34:12; Yer 25:22; Law 26:33
[i]**31:11** Kut 6:6; Isa 44:23; Za 142:6; 9:16
[j]**31:12** Eze 40:2; Mik 4:1; Yoe 3:18; Hes 18:12; Hos 2:21-22; Wim 4:15; Yn 16:22; Isa 58:11; Wim 4:15; Isa 30:19

13 [a]Kisha wanawali watacheza na
kufurahi,
vijana waume na wazee pia.
Nitageuza maombolezo yao kuwa
furaha,
nitawapa faraja na furaha badala
ya huzuni.
14 [b]Nitawashibisha makuhani kwa
wingi,
nao watu wangu watajazwa kwa
ukarimu wangu,"
asema BWANA.

15 [c]Hili ndilo asemalo BWANA:

"Sauti imesikika huko Rama,
maombolezo na kilio kikubwa,
Raheli akiwalilia watoto wake
na anakataa kufarijiwa,
kwa sababu watoto wake hawako
tena."

16 [d]Hili ndilo asemalo BWANA:

"Izuie sauti yako kulia,
na macho yako yasitoe machozi,
kwa kuwa kazi yako itapata
thawabu,"
asema BWANA.
"Watarudi kutoka nchi ya adui.
17 Kwa hiyo kuna tumaini kwa siku
zijazo,"
asema BWANA.
"Watoto wako watarudi nchi yao
yenyewe.

18 [e]"Hakika nimeyasikia maombolezo
ya Efraimu:
'Ulinirudi kama ndama mkaidi,
nami nimekubali kutii.
Unirudishe, nami nitarudi,
kwa sababu wewe ndiwe BWANA,
Mungu wangu.
19 [f]Baada ya kupotea, nilitubu;
baada ya kuelewa, nilijipiga kifua.
Niliaibika na kuona haya
kwa sababu niliibeba aibu ya
ujana wangu.'
20 [g]Je, Efraimu si mwanangu mpendwa,
mtoto ninayependezwa naye?
Ingawa mara kwa mara ninanena
dhidi yake,
bado ninamkumbuka.
Kwa hiyo moyo wangu unamwonea
shauku,
nina huruma kubwa kwa ajili
yake,"
asema BWANA.

21 [h]"Weka alama za barabara,
weka vibao vya kuelekeza.
Zingatia vyema njia kuu,
barabara ile unayoipita.
Rudi, ee Bikira Israeli,
rudi kwenye miji yako.
22 [i]Utatangatanga hata lini,
ee binti usiye mwaminifu?
BWANA ameumba kitu kipya
duniani:
mwanamke atamlinda
mwanaume."

23 [j]Hili ndilo BWANA Mwenye Nguvu
Zote, Mungu wa Israeli, asemalo,
"Nitakapowarudisha toka nchi ya
kutekwa kwenu, watu walio katika nchi
ya Yuda na miji yake kwa mara nyingine
tena watatumia maneno haya: 'BWANA
akubariki, ee makao ya haki, ee mlima
mtakatifu.' 24 [k]Watu wataishi pamoja
katika Yuda na miji yake yote, wakulima
na wote wanaohamahama na mifugo

[a]**31:13** Isa 61:3; Za 30:11; Isa 51:11
[b]**31:14** Law 7:35-36; Za 36:8; Isa 30:23
[c]**31:15** Yos 18:25; Mwa 37:35; Yer 10:20; Mt 2:17-18; Ay 7:21
[d]**31:16** Za 30:5; Isa 25:8; Rut 2:12; Eze 11:17-18; 2Nya 15:7; Yer 30:3; Isa 30:19
[e]**31:18** Ay 5:17; Hos 4:16; 10:11; Za 80:3-4; Mao 5:21; Yer 50:11
[f]**31:19** Za 95:10; Eze 36:31; 21:12; Lk 18:13; Yer 8:4; Ezr 9:6; Za 25:7
[g]**31:20** Isa 44:21; Hos 4:4; Mik 7:18; 1Fal 3:26; Mao 3:33; Isa 55:7
[h]**31:21** Isa 35:8; Yer 50:5; Isa 52:11; Yer 3:12; Eze 21:19
[i]**31:22** Yer 2:23; Hos 4:16; Isa 43:19; Kum 32:10
[j]**31:23** Yer 30:18; Isa 1:26; Zek 8:3; Mwa 28:3; Hes 6:24; Isa 2:2; Za 48:1
[k]**31:24** Yer 33:12, 18; Zek 8:4-8; Yer 30:18

yao. 25 [a]Nitawaburudisha waliochoka na
kuwatuliza walio na huzuni."
26 Kwa jambo hili niliamka na kuangalia
pande zote. Usingizi wangu ulikuwa mtamu
kwangu.
27 [b]BWANA asema, "Siku zinakuja,
nitakapoongeza idadi ya watu, na kuzidisha
hesabu ya mifugo katika nyumba ya
Israeli na nyumba ya Yuda. 28 [c]Kama vile
nilivyowaangalia ili kung'oa na kubomoa,
kuharibu, kuangamiza na kuleta maafa juu
yao, vivyo hivyo nitawaangalia ili kujenga
na kupanda," asema BWANA. 29 [d]"Katika
siku hizo, watu hawatasema tena,

" 'Baba wamekula zabibu chachu,
nayo meno ya watoto yakatiwa
ganzi.'

30 [e]Badala yake, kila mmoja atakufa kwa
ajili ya dhambi zake mwenyewe; yeyote
alaye zabibu chachu, meno yake mwenyewe
yatatiwa ganzi.

31 [f]"Siku zinakuja," asema BWANA,
"nitakapofanya agano jipya
na nyumba ya Israeli
na nyumba ya Yuda.
32 [g]Halitafanana na agano
nililofanya na baba zao
wakati nilipowashika mkono
kuwaongoza watoke Misri,
kwa sababu walivunja agano langu,
ijapokuwa nilikuwa mume kwao,"
asema BWANA.
33 [h]"Hili ndilo agano nitakalofanya na
nyumba ya Israeli
baada ya siku zile," asema
BWANA.
"Nitaweka sheria yangu katika nia
zao,
na kuiandika mioyoni mwao.
Nitakuwa Mungu wao,
nao watakuwa watu wangu.
34 [i]Mtu hatamfundisha tena jirani yake,
wala mtu kumfundisha ndugu
yake akisema, 'Mjue BWANA
Mungu,'
kwa sababu wote watanijua mimi,
tangu aliye mdogo kabisa kwao,
hadi aliye mkuu sana,"
asema BWANA.
"Kwa sababu nitasamehe uovu wao,
wala sitazikumbuka dhambi zao
tena."

35 [j]Hili ndilo asemalo BWANA,

yeye aliyeweka jua
liwake mchana,
yeye anayeamuru mwezi na nyota
kung'aa usiku,
yeye aichafuaye bahari
ili mawimbi yake yangurume;
BWANA Mwenye Nguvu Zote ndilo
jina lake:
36 [k]"Ikiwa amri hizi zitaondoka
machoni pangu,"
asema BWANA,
"ndipo wazao wa Israeli watakoma
kuwa taifa mbele yangu daima."

37 [l]Hili ndilo asemalo BWANA:

"Ikiwa mbingu zilizo juu zitaweza
kupimika
na misingi ya dunia chini
ikaweza kuchunguzwa,
ndipo nitakapowakataa wazao wote
wa Israeli
kwa sababu ya yote
waliyoyatenda,"
asema BWANA.

---

[a]**31:25** Yn 4:14; Isa 40:29
[b]**31:27** Eze 36:9-11; Hos 2:23; Yer 16:14
[c]**31:28** Yer 18:8; 44:27; Kum 30; 9; Amo 9:14; Ay 29:2; Eze 36:10-11; Yer 1:10
[d]**31:29** Mwa 9:25; Kum 24:16; Eze 18:2; Mao 5:7
[e]**31:30** 2Fal 14:6; Gal 6:7; Isa 3:11
[f]**31:31** Kum 29:14; Ebr 8:8-12; Yer 33:14; Lk 22:20; Isa 42:6; 54:10; Ebr 10:16-17
[g]**31:32** Kut 24:8; Kum 5:3; 1:31; Yer 11:4; Isa 54:5
[h]**31:33** Kum 6:6; 2Kor 3:3; Yer 24:7; Ebr 10:16; Za 40:8; Kut 4:15
[i]**31:34** 1Yn 2:27; Yn 6:45; Isa 54:13; Za 85:2; Mik 7:19; Rum 11:27; Isa 11:9
[j]**31:35** Za 136:7-9; Mwa 1; 16; Yer 10:16; Kut 14:21; Za 93:3
[k]**31:36** Ay 38:33; Isa 54:9-10; Za 89:36-37; Yer 33:20-26
[l]**31:37** Ay 38:5; Yer 33:22, 24, 26; Rum 11:1-5

38 [a]“Siku zinakuja,” asema BWANA,
“wakati mji huu utajengwa upya kwa ajili
yangu, kuanzia mnara wa Hananeli hadi
Lango la Pembeni. 39 [b]Kamba ya kupimia
itaanzia hapo kuendelea hadi kwenye kilima
cha Garebu, na kisha kugeuka kuelekea
Goa. 40 [c]Bonde lote watupwapo maiti na
majivu pia na matuta yote kutoka Bonde la
Kidroni upande wa mashariki hadi pembe
ya Lango la Farasi, itakuwa takatifu kwa
BWANA. Kamwe mji huu hautang’olewa
tena wala kubomolewa.”

*Yeremia Anunua Shamba*

32 [d]Hili ndilo neno lililomjia Yeremia
kutoka kwa BWANA, katika mwaka wa
kumi wa utawala wa Sedekia mfalme wa
Yuda, ambao ulikuwa mwaka wa kumi na
nane wa utawala wa Mfalme Nebukadneza.
2 [e]Wakati huo jeshi la mfalme wa Babeli
lilikuwa limeuzunguka mji wa Yerusalemu,
naye nabii Yeremia alikuwa amezuiliwa
katika ua wa walinzi katika jumba la
kifalme la Yuda.
3 [f]Basi Sedekia mfalme wa Yuda
alikuwa amemfunga huko akisema, “Kwa
nini unatabiri hivyo? Wewe unasema,
‘Hili ndilo asemalo BWANA: Ninakaribia
kuutia mji huu mkononi mwa mfalme wa
Babeli, naye atauteka. 4 [g]Sedekia mfalme
wa Yuda hataweza kuponyoka mikononi
mwa Wakaldayo, lakini kwa hakika
atatiwa mikononi mwa mfalme wa Babeli,
naye atazungumza naye ana kwa ana na
kumwona kwa macho yake mwenyewe.
5 [h]Atamchukua Sedekia hadi Babeli, mahali
atakapoishi mpaka nitakapomshughulikia,
asema BWANA. Kama utapigana dhidi ya
Wakaldayo, hutashinda.’ ”
6 Yeremia akasema, “Neno la BWANA
lilinijia kusema: 7 [i]Hanameli mwana wa
Shalumu mjomba wako atakuja kwako
na kusema, ‘Nunua shamba langu huko
Anathothi, kwa sababu wewe kama
jamaa ya karibu ni haki na wajibu wako
kulinunua.’
8 “Kisha, kama BWANA alivyosema,
binamu yangu Hanameli alinijia katika
ua wa walinzi na kusema: ‘Nunua shamba
langu lililoko Anathothi katika nchi
ya Benyamini. Kwa kuwa ni haki yako
kulikomboa na kulimiliki, jinunulie.’
“Nilijua kwamba hili lilikuwa neno la
BWANA. 9 [j]Hivyo nikalinunua shamba hilo
lililoko Anathothi kutoka kwa binamu
yangu Hanameli, nami nikampimia shekeli
kumi na saba[k] za fedha. 10 [l]Nikatia sahihi
na kuweka muhuri hati ya kumiliki,
nikaweka mashahidi, na kupima ile fedha
kwenye mizani. 11 Nikachukua ile hati ya
kununulia, nakala iliyotiwa muhuri yenye
makubaliano na masharti, pia pamoja
na ile nakala isiyo na muhuri, 12 [m]nami
nikampa Baruku mwana wa Neria, mwana
wa Maaseya, hati hii mbele ya binamu
yangu Hanameli, na mbele ya mashahidi
waliokuwa wameweka sahihi kwenye hati
hii na mbele ya Wayahudi wote waliokuwa
wameketi katika ua wa walinzi.
13 “Nilimpa Baruku maelezo haya mbele
yao: 14 [n]‘Hili ndilo asemalo BWANA Mwenye
Nguvu Zote, Mungu wa Israeli: Chukua
hati hizi, yaani nakala zote zenye muhuri
na zisizo na muhuri za hati ya kununulia,
na uziweke kwenye gudulia la udongo wa
mfinyanzi ili zidumu kwa muda mrefu.
15 [o]Kwa kuwa hili ndilo asemalo BWANA
Mwenye Nguvu Zote, Mungu wa Israeli:

[a]**31:38** Yer 30:18; Neh 3:1; 2Nya 25:23; Zek 14:10; Yer 24:6; 2Fal 14:13
[b]**31:39** 1Fal 7:23
[c]**31:40** Yer 2:23; 7:31-32; 1Sam 15:23; Yn 18:1; 2Fal 11:16; Yoe 3:17; Zek 14:21
[d]**32:1** 2Fal 25:1; Yer 25:1; 39:1
[e]**32:2** Neh 3:25; Yer 37:21; Mt 5:12; Za 88:8
[f]**32:3** Yer 26:8-9; 21; 4; 34:2-4
[g]**32:4** Yer 21:7; 52:9; 44:30; 34:21; 38:18, 23; 39:5-7
[h]**32:5** Yer 39:7; Eze 12:13; Mao 1:14; Mit 21:30; Yer 21:4; 2Fal 25:7
[i]**32:7** Law 25:24-32; Rut 4:3-4; Mt 27:10; Yos 21:18
[j]**32:9** Mwa 23:16; Yer 37:12
[k]9 Shekeli 17 za fedha ni sawa na gramu 200.
[l]**32:10** Rut 4:9; Isa 8:2; Mwa 23:20
[m]**32:12** Yer 36:4; 43:3-6; 51:59
[n]**32:14** Isa 8:16
[o]**32:15** Eze 28:26; Amo 9:14-15; Yer 30:18; Isa 44:26

Nyumba, mashamba na mashamba ya
mizabibu yatanunuliwa tena katika nchi
hii.’

16 “Baada ya kumkabidhi Baruku mwana
wa Neria hii hati ya kununulia, nilimwomba
Bwana:

> 17 [a]“Ee Bwana Mwenyezi, umeumba
> mbingu na nchi kwa uwezo wako mkuu
> na kwa mkono ulionyooshwa. Hakuna
> jambo lililo gumu usiloliweza. 18 [b]Wewe
> huonyesha upendo kwa maelfu, lakini
> huleta adhabu kwa ajili ya dhambi za
> baba mapajani mwa watoto wao baada
> yao. Ee Mungu mkuu na mwenye
> uweza, ambaye jina lako ni Bwana
> Mwenye Nguvu Zote, 19 [c]makusudi
> yako ni makuu, na matendo yako ni
> yenye uwezo. Macho yako yanaona
> njia zote za wanadamu, nawe humlipa
> kila mmoja kulingana na mwenendo
> wake, na kama yanavyostahili matendo
> yake. 20 [d]Ulitenda ishara za miujiza na
> maajabu huko Misri, na umeyaendeleza
> mpaka leo, katika Israeli na miongoni
> mwa wanadamu wote, nawe
> umejulikana na kufahamika hivyo
> mpaka leo. 21 [e]Uliwatoa watu wako
> Israeli kutoka Misri kwa ishara na
> maajabu, kwa mkono wenye nguvu na
> ulionyooshwa na kwa matisho makuu.
> 22 [f]Uliwapa nchi hii uliyokuwa umeapa
> kuwapa baba zao, nchi inayotiririka
> maziwa na asali. 23 [g]Waliingia na
> kuimiliki, lakini hawakukutii wala
> kuifuata sheria yako. Hawakufanya
> kile ulichowaamuru kufanya. Hivyo
> ukaleta maafa haya yote juu yao.
>
> 24 [h]“Tazama jinsi tumezungukwa na
> jeshi ili kuuteka mji huu. Kwa sababu
> ya upanga, njaa na tauni, mji utatiwa
> mikononi mwa Wakaldayo ambao
> wanaushambulia. Ulilosema limetokea
> kama vile unavyoona sasa. 25 Ingawa
> mji utatiwa mikononi mwa Wakaldayo,
> wewe, Ee Bwana Mwenyezi,
> uliniambia, ‘Nunua shamba kwa fedha,
> na jambo hilo lishuhudiwe.’ ”

26 Ndipo neno la Bwana likamjia
Yeremia kusema: 27 [i]“Mimi ndimi Bwana,
Mungu wa wote wenye mwili. Je, kuna
jambo lolote lililo gumu nisiloliweza?
28 [j]Kwa hiyo, hili ndilo asemalo Bwana:
Ninakaribia kuutia mji huu mikononi mwa
Wakaldayo, na mwa Nebukadneza mfalme
wa Babeli ambaye atauteka. 29 [k]Wakaldayo
ambao wanaushambulia mji huu watakuja
na kuuchoma moto na kuuteketeza, pamoja
na nyumba ambamo watu wamenikasirisha
kwa kumfukizia Baali uvumba katika
mapaa na kumimina sadaka za vinywaji
kwa miungu mingine.

30 [l]“Watu wa Israeli na wa Yuda
hawakufanya kitu kingine ila uovu mbele
zangu tangu ujana wao. Naam, watu
wa Israeli hawakufanya kitu kingine ila
kunikasirisha kwa kazi ambazo mikono
yao imetengeneza, asema Bwana.
31 [m]Tangu siku ulipojengwa hadi sasa, mji
huu umenikasirisha na kunighadhibisha
kiasi kwamba ni lazima niuondoe
machoni pangu. 32 [n]Watu wa Israeli na wa
Yuda wamenikasirisha kwa uovu wote
waliofanya: wao, wafalme wao na maafisa
wao, makuhani wao na manabii wao,
watu wa Yuda na wakazi wa Yerusalemu.

---

[a]**32:17** Kum 9:29; Kut 20:5; Za 102:25; 2Fal 3:18; Mwa 32:9-12; Mt 19:26; 2Fal 19:15
[b]**32:18** Kum 5:9-10; Eze 20:5; Kut 20:6; Za 109:14; Yer 10:16; Za 79:12
[c]**32:19** Isa 28:29; Ay 34:11, 21; Mit 5:21; Dan 2:20; Mt 16:27; Ay 12:13; 14:16
[d]**32:20** Kut 9:16; Isa 63:12; Kut 3:20; Ay 9:10; Isa 55:13; Yer 13:11
[e]**32:21** 1Nya 17:21; Kut 6:6; Kum 26:8; 2Sam 7:23; Dan 9:15; Yer 6:12; Kum 5:15
[f]**32:22** Kut 3:8; Eze 20:6
[g]**32:23** Za 78:54-55; Neh 9:26; Dan 9:10-14; Kum 28:64; Za 44:2; Kut 16:28; Yer 11:8
[h]**32:24** Yer 14:12; Yos 23:15; Kum 4:25-26; 2Sam 20:15; Yer 6:6; Kum 28:2
[i]**32:27** Hes 16:22; Mwa 18:14; 2Fal 3:18
[j]**32:28** 2Nya 36:17; Yer 21:10
[k]**32:29** Yer 19:13; 52:13; 44:18; 7:9
[l]**32:30** Za 25:7; Yer 22:21; 8:19; 25:7
[m]**32:31** 2Fal 23:27; 24:3; Sef 3:1; Mt 23:37; 2Fal 21:4-5; 1Fal 11:7-8
[n]**32:32** Isa 1:4-6; Dan 9:8; 1Fal 14:9; Yer 2:26; 44:9

33 [a]Walinigeuzia visogo vyao, wala si
nyuso zao. Ingawa niliwafundisha tena
na tena, hawakupenda kusikiliza wala
kuitikia adhabu. 34 [b]Waliweka miungu
yao ya kuchukiza sana katika nyumba
iitwayo kwa Jina langu na kuinajisi.
35 [c]Wakajenga mahali pa juu pa kuabudia
miungu kwa ajili ya Baali katika Bonde la
Ben-Hinomu, ambapo walitoa wana wao
na binti zao kafara kwa Moleki, ingawa
kamwe sikuamuru, wala halikuingia akilini
mwangu, kwamba watafanya chukizo kama
hilo na kumfanya Yuda atende dhambi.
36 “Mnasema kuhusu mji huu, ‘Kwa
upanga, njaa na tauni, mji utatiwa mkononi
mwa mfalme wa Babeli,’ lakini hili ndilo
BWANA, Mungu wa Israeli asemalo:
37 [d]Hakika nitawakusanya kutoka nchi zote
nilizowafukuzia katika hasira yangu kali na
ghadhabu yangu kuu, nitawarudisha mahali
hapa na kuwaruhusu waishi kwa salama.
38 [e]Watakuwa watu wangu, nami nitakuwa
Mungu wao. 39 [f]Nitawapa moyo mmoja na
kutenda pamoja, ili kwamba waniche daima
kwa mema yao wenyewe na kwa mema
ya watoto wao baada yao. 40 [g]Nitafanya
nao agano la milele: Kamwe sitaacha
kuwatendea mema, nami nitawavuvia
kunicha mimi, ili kamwe wasigeukie mbali
nami. 41 [h]Nitafurahia kuwatendea mema,
na kwa hakika nitawapanda katika nchi hii
kwa moyo wangu wote na roho yangu yote.
42 [i]“Hili ndilo asemalo BWANA: Kama
nilivyoleta maafa haya makubwa kwa watu
hawa, ndivyo nitakavyowapa mafanikio
niliyowaahidi. 43 Kwa mara nyingine tena
mashamba yatanunuliwa katika nchi hii
ambayo mlisema, ‘Imekuwa ukiwa, isiyofaa,
isiyo na watu wala wanyama, kwa sababu
imetiwa mikononi mwa Wakaldayo.’
44 [j]Mashamba yatanunuliwa kwa fedha, na
hati zitatiwa sahihi, zitatiwa muhuri na
kushuhudiwa katika nchi ya Benyamini,
katika vijiji vinavyoizunguka Yerusalemu,
katika miji ya Yuda na katika miji ya nchi
ya vilima, sehemu za magharibi katika
miji ya tambarare na katika Negebu, kwa
sababu nitarudisha tena mafanikio yao,[k]
asema BWANA.”

*Ahadi Ya Kurudishwa*

33 [l]Wakati Yeremia alipokuwa angali
amefungwa kwenye ua wa walinzi,
neno la BWANA lilimjia mara ya pili
kusema: 2 [m]“Hili ndilo BWANA asemalo,
yeye aliyeumba dunia, BWANA aliyeifanya
na kuithibitisha, BWANA ndilo jina lake:
3 [n]‘Niite nami nitakuitikia na kukuambia
mambo makuu na yasiyochunguzika,
usiyoyajua.’ 4 [o]Kwa maana hili ndilo BWANA,
Mungu wa Israeli, asemalo kuhusu nyumba
katika mji huu na majumba ya kifalme ya
Yuda yaliyobomolewa ili yatumiwe dhidi
ya kule kuzungukwa na jeshi na upanga
5 [p]katika kupigana na Wakaldayo: ‘Zitajazwa
na maiti za watu nitakaowachinja katika
hasira na ghadhabu yangu. Nitauficha uso
wangu kwa sababu ya maovu yake yote.
6 [q]“ ‘Hata hivyo, nitauletea afya na
uponyaji, nitawaponya watu wangu na
kuwafanya wafurahie amani tele na salama.
7 [r]Nitawarudisha Yuda na Israeli kutoka nchi
ya kutekwa kwao, na kuwajenga tena kama

[a]**32:33** 1Fal 14:9; Za 14:3; Kum 4:5; Isa 28:9; Yer 7:13, 28; 2:27; Eze 8:16; Zek 7:11
[b]**32:34** Yer 7:30; Eze 8:3-16
[c]**32:35** Law 18:21; Yer 7:31; 2Fal 23:10; Yer 19:5; 25:7
[d]**32:37** Isa 11:12; Yer 23:3-6; Law 25:18; Kum 30:3; Eze 34:28; 39:26; Yer 21:5
[e]**32:38** Yer 24:7; 2Kor 6:16
[f]**32:39** Eze 11:19; Yn 17:21; 2Nya 30:12; Mdo 4:32; Kum 6:24; 10:16; Za 86:11
[g]**32:40** Mwa 9:16; Isa 55:3; Yer 24; 7; Isa 42:6; Kum 4:10
[h]**32:41** Kum 28:3-12; Yer 24:6; Kum 30; 9; Amo 9:15; Yer 31:28; Isa 62:4; Mik 7:18
[i]**32:42** Yer 29:10; 31:28; Mao 3:38
[j]**32:44** Yer 17:26; Ezr 9:9; Yer 33:7, 11, 26; Rut 4:9; Isa 8:2; Za 14:7
[k]44 Au: nitawarudisha tena kutoka utumwani.
[l]**33:1** Yer 32:2; 37:21; 38:28; Za 88:8; Yer 13:3
[m]**33:2** Yer 10:16; Za 136:6; Kut 3:15; 15:3
[n]**33:3** Mwa 18:17; Yer 29:12; Isa 55:6; Ay 28:11
[o]**33:4** 2Fal 25:1; Eze 4:2; 26:8; Hab 1:10; Yer 32:24
[p]**33:5** Yer 21:4-7; Kum 31:17; Isa 8:17
[q]**33:6** Kum 32:39; Isa 30:26; 9:6
[r]**33:7** Yer 32:44; Eze 39:25; Amo 9:14; Isa 1:26; Yer 24:6; 30:3

walivyokuwa hapo awali. 8 [a]Nitawatakasa
dhambi zote walizofanya dhidi yangu, na
nitawasamehe dhambi zote za uasi dhidi
yangu. 9 [b]Kisha mji huu utaniletea utukufu,
furaha, sifa na heshima mbele ya mataifa
yote ya dunia yatakayosikia mambo yote
mazuri ninayoufanyia. Nao watashangaa na
kutetemeka kwa ajili ya wingi wa mafanikio
na amani nitakayoupatia.'

10 [c]"Hili ndilo asemalo BWANA: 'Mnasema
kuhusu mahali hapa kwamba, "Ni mahali
palipoachwa ukiwa, pasipo na wanadamu
wala wanyama." Lakini katika miji ya
Yuda na barabara za Yerusalemu ambazo
zimeachwa, ambazo hazikaliwi na
wanadamu wala wanyama, huko kutasikika
kwa mara nyingine 11 [d]sauti za shangwe na
furaha, sauti za bibi na bwana arusi, na
sauti za wale waletao sadaka za shukrani
katika nyumba ya BWANA, wakisema,

" ' "Mshukuruni BWANA Mwenye
Nguvu Zote,
kwa maana BWANA ni mwema;
upendo wake wadumu milele."

Kwa kuwa nitairudishia nchi baraka kama
zilivyokuwa hapo awali,' asema BWANA.

12 [e]"Hili ndilo asemalo BWANA Mwenye
Nguvu Zote: 'Mahali hapa, ambapo ni ukiwa,
pasipo na wanadamu wala wanyama: katika
miji yake, patakuwepo tena malisho kwa
ajili ya wachungaji kupumzisha makundi
yao ya kondoo. 13 [f]Katika miji ya nchi ya
vilima, ya vilima vya magharibi na ya
Negebu, katika nchi ya Benyamini, katika
vijiji vinavyoizunguka Yerusalemu na
katika miji ya Yuda, makundi ya kondoo
yatapita tena chini ya mkono wa yeye
ayahesabuye,' asema BWANA.

14 [g]" 'Siku zinakuja,' asema BWANA,
'wakati nitakapotimiza ahadi yangu ya
rehema niliyoifanya kwa nyumba ya Israeli
na kwa nyumba ya Yuda.

15 [h]" 'Katika siku hizo na wakati huo
nitalifanya Tawi la haki lichipuke
kutoka ukoo wa Daudi,
naye atafanya lile lililo haki na sawa
katika nchi.
16 [i]Katika siku hizo, Yuda ataokolewa
na Yerusalemu ataishi salama.
Hili ndilo jina atakaloitwa:
BWANA Haki Yetu.'

17 [j]Kwa maana hili ndilo asemalo BWANA:
'Daudi kamwe hatakosa mtu wa kukalia
kiti cha enzi cha nyumba ya Israeli, 18 [k]wala
hata makuhani, ambao ni Walawi, kamwe
hawatakosa mtu wa kusimama mbele zangu
daima ili kutoa sadaka za kuteketezwa,
ili kuteketeza sadaka ya nafaka na kutoa
dhabihu.' "

19 Neno la BWANA likamjia Yeremia
kusema: 20 [l]"Hili ndilo asemalo BWANA:
'Ikiwa mtaweza kuvunja agano langu
kuhusu usiku na mchana, ili usiku na
mchana visiwepo kwa nyakati zake,
21 [m]basi agano langu na Daudi mtumishi
wangu, na agano langu na Walawi ambao
ni makuhani wanaohudumu mbele zangu,
linaweza kuvunjwa, na Daudi hatakuwa
tena na mzao wa kutawala katika kiti chake
cha enzi. 22 [n]Nitawafanya wazao wa Daudi
mtumishi wangu na Walawi wanaohudumu
mbele zangu wengi, wasioweza kuhesabika
kama nyota za angani, tena wasiopimika
kama mchanga wa ufuoni mwa bahari.' "

23 Neno la BWANA likamjia Yeremia

---

[a]**33:8** Law 16:30; Ebr 9:13-14; 2Sam 24:14; Mik 7:18; Yer 31:34
[b]**33:9** Isa 60:18; Yer 13:11; Isa 64:2; Yer 3:17; 1Yn 1:7-9; Isa 55:13
[c]**33:10** Yer 32:43; 9:11
[d]**33:11** Za 51:8; 24:8; Law 7:12; 2Nya 5:13; Za 25:8; 100:4-5; 14:7
[e]**33:12** Yer 32:43; Isa 65:10; Eze 34:11-15
[f]**33:13** Yer 32:43; Isa 65:10; Eze 34:11-15
[g]**33:14** Kum 28:1-14; Yos 23:15; Yer 29:10
[h]**33:15** Isa 4:2; Za 72:2; Isa 11:1; 2Sam 7:12
[i]**33:16** Isa 45:17; 1Kor 1:30; Zek 8:3, 16; Sef 3:13; Eze 48:35; Yer 3:17; Isa 59:14; Yer 32:37
[j]**33:17** 2Sam 7:13; 2Nya 7:18; Za 89:29-37
[k]**33:18** Kum 18:1; Ebr 13:15; Hes 25:11-13; Ebr 7:17-22
[l]**33:20** Za 89:36; Mwa 8:22; Isa 54:9; Mwa 1:14
[m]**33:21** Za 89:34; 2Sam 7:13-18; 2Nya 7:18
[n]**33:22** Mwa 15:5; Hos 1:10; Mwa 13:16; Yer 30:19; Mwa 12:2

kusema: 24 [a]“Je, hujasikia kwamba watu
hawa wanasema, ‘Bwana amezikataa
zile falme mbili alizozichagua?’ Kwa
hiyo wamewadharau watu wangu, na
hawawaoni tena kama taifa. 25 [b]Hili ndilo
asemalo Bwana: ‘Kama sijathibitisha agano
langu na usiku na mchana, na kuziweka
wakfu sheria za mbingu na nchi, 26 [c]basi
nitawakataa wazao wa Yakobo na Daudi
mtumishi wangu, na sitachagua mmoja
wa wanawe kutawala juu ya wazao wa
Abrahamu, Isaki na Yakobo. Kwa maana
nitawarudisha kutoka nchi ya kutekwa
kwao na kuwaonea huruma.’ ”

*Onyo Kwa Sedekia*

34 [d]Wakati Nebukadneza mfalme wa
Babeli na jeshi lake lote, pamoja
na falme zote na mataifa katika himaya
aliyotawala walipokuwa wakipigana
dhidi ya Yerusalemu pamoja na miji yote
inayoizunguka, neno hili lilimjia Yeremia
kutoka kwa Bwana: 2 [e]“Hili ndilo asemalo
Bwana, Mungu wa Israeli, kusema: Nenda
kwa Sedekia mfalme wa Yuda umwambie,
‘Hili ndilo asemalo Bwana: Ninakaribia
kuutia mji huu mikononi mwa mfalme
wa Babeli, naye atauteketeza kwa moto.
3 [f]Hutaweza kuepuka mkono wake, bali
hakika utatekwa na kukabidhiwa kwake.
Utamwona mfalme wa Babeli kwa macho
yako mwenyewe, naye atazungumza nawe
ana kwa ana. Nawe utakwenda Babeli.
4 [g]“ ‘Lakini sikia ahadi ya Bwana, ee
Sedekia mfalme wa Yuda. Hili ndilo
asemalo Bwana kukuhusu: Hutakufa
kwa upanga, 5 [h]utakufa kwa amani.
Kama vile watu walivyowasha moto
wa maziko kwa heshima ya baba zako,
wafalme waliokutangulia, ndivyo watu
watakavyowasha moto kwa heshima
yako na kuomboleza, wakisema: “Ole, Ee
Bwana!” Mimi mwenyewe ninaweka ahadi
hii, asema Bwana.’ ”
6 Ndipo nabii Yeremia akamwambia
Sedekia mfalme wa Yuda mambo haya
yote huko Yerusalemu, 7 [i]wakati jeshi la
mfalme wa Babeli lilipokuwa likipigana
dhidi ya Yerusalemu na miji mingine ya
Yuda ambayo bado ilikuwa imara, yaani
Lakishi na Azeka. Hii ilikuwa miji pekee
yenye ngome iliyobaki katika Yuda.

*Uhuru Kwa Watumwa*

8 [j]Hili ndilo neno lililomjia Yeremia
kutoka kwa Bwana, baada ya Mfalme
Sedekia kufanya agano na watu wote
huko Yerusalemu ili kutangaza uhuru
kwa watumwa. 9 [k]Kila mmoja alipaswa
kuwaacha huru watumwa wake wa
Kiebrania, wanawake na wanaume. Hakuna
yeyote aliyeruhusiwa kumshikilia Myahudi
mwenzake kama mtumwa. 10 Kwa hiyo
maafisa wote na watu walioingia katika
agano hili wakakubali kwamba watawaacha
huru watumwa wao wa kiume na wa kike,
na hawatawashikilia tena kama watumwa.
Wakakubali na wakawaacha huru. 11 Lakini
baadaye wakabadili mawazo yao, na
kuwarudisha wale watumwa waliokuwa
wamewaacha huru, wakawafanya tena
watumwa.
12 Ndipo neno la Bwana likamjia Yeremia
kusema: 13 [l]“Hili ndilo asemalo Bwana,
Mungu wa Israeli: Nilifanya agano na baba
zenu nilipowatoa Misri, kutoka nchi ya
utumwa. Nilisema, 14 [m]‘Kila mwaka wa saba,
kila mmoja wenu ni lazima amwache huru
mtumwa ambaye ni Mwebrania mwenzenu
aliyejiuza kwenu. Baada ya kukutumikia
kwa miaka sita, ni lazima umwache
huru aende zake.’ Hata hivyo baba zenu

[a]**33:24** Eze 37:22; Neh 4:4; Yer 30:17; Eze 36:20
[b]**33:25** Mwa 1:18; Yer 31:35-36; Za 74:16-17; 148:6
[c]**33:26** Law 26:44; Yer 31:37; Isa 14:1; Zek 10:6; Za 14:7; Yer 30:18
[d]**34:1** Yer 27:7; 2Fal 25:1; Yer 39:1; Dan 2:37
[e]**34:2** 2Nya 36:11; Yer 32:29; 37:8
[f]**34:3** Yer 32:4; 21:7; 2Fal 25:7
[g]**34:4** Yer 52:11
[h]**34:5** 2Nya 16:14
[i]**34:7** Yos 10:3-10; 2Nya 11:9; 2Fal 18:13
[j]**34:8** 2Fal 11:17; Kut 21:2; Neh 5:5-8; Law 25:39-41
[k]**34:9** Law 25:39-46; Kum 15:12-18; Neh 5:11
[l]**34:13** Kut 24:8; Kum 15:15
[m]**34:14** Kut 21:2; Law 25:39; Kum 15:12; 2Fal 17:14; Yer 7:26

hawakunisikiliza wala kunijali. 15 [a]Hivi
karibuni tu mlitubu na kufanya yaliyo
sawa machoni pangu: Kila mmoja wenu
aliwatangazia uhuru Waebrania wake.
Hata mlifanya agano mbele zangu ndani ya
nyumba iitwayo kwa Jina langu. 16 [b]Lakini
sasa mmegeuka na kulinajisi jina langu.
Kila mmoja wenu amemrudisha mtumwa
wa kiume na wa kike ambao mlikuwa
mmewaacha huru waende zao walikotaka.
Mmewalazimisha kuwa watumwa wenu
tena.
17 [c]"Kwa hiyo, hili ndilo asemalo BWANA:
Hamkunitii mimi. Hamkutangaza uhuru kwa
ndugu zenu. Hivyo sasa, ninawatangazia
ninyi 'uhuru,' asema BWANA: 'uhuru' ili
kuanguka kwa upanga, tauni na njaa.
Nitawafanya mwe chukizo kwa falme zote
za dunia. 18 [d]Watu waliovunja agano langu,
na ambao hawakutunza masharti ya agano
walilofanya mbele zangu, nitawafanya
kama ndama waliyemkata vipande viwili,
kisha wakatembea kati ya vile vipande
vya huyo ndama. 19 [e]Viongozi wa Yuda
na Yerusalemu, maafisa wa mahakama,
makuhani na watu wote wa nchi waliopita
kati ya vile vipande vya ndama, 20 [f]nitawatia
mikononi mwa adui zao wanaotafuta uhai
wao. Maiti zao zitakuwa chakula cha ndege
wa angani na wanyama wa nchi.
21 [g]"Nitamtia Sedekia mfalme wa Yuda
na maafisa wake mikononi mwa adui
zao wanaotafuta uhai wao, kwa jeshi la
mfalme wa Babeli, lililokuwa limeondoka
kwenu. 22 [h]Nitatoa amri, asema BWANA,
nami nitawarudisha tena katika mji huu.
Watapigana dhidi yake, wautwae na
kuuteketeza kwa moto. Nami nitaiangamiza
miji ya Yuda hivyo pasiwe na yeyote
atakayeweza kuishi humo."

*Warekabi Wasifiwa*

35 [i]Hili ndilo neno lililomjia Yeremia
kutoka kwa BWANA, wakati wa
utawala wa Yehoyakimu mwana wa Yosia
mfalme wa Yuda: 2 [j]"Nenda kwa jamaa ya
Warekabi, uwaalike waje kwenye moja
ya vyumba vya pembeni vya nyumba ya
BWANA, na uwape divai wanywe."
3 Basi nikaenda kumwita Yaazania mwana
wa Yeremia, mwana wa Habazinia, na
ndugu zake na wanawe wote, yaani jamaa
nzima ya Warekabi. 4 [k]Nikawaleta katika
nyumba ya BWANA, ndani ya chumba cha
wana wa Hanani mwana wa Igdalia mtu
wa Mungu. Kilikuwa karibu na chumba cha
maafisa, ambacho kilikuwa juu ya kile cha
Maaseya mwana wa Shalumu, aliyekuwa
bawabu. 5 Kisha nikaweka mabakuli
yaliyojaa divai na baadhi ya vikombe
mbele ya watu wa jamaa ya Warekabi na
kuwaambia, "Kunyweni divai."
6 [l]Lakini wao wakajibu, "Sisi hatunywi
divai, kwa sababu baba yetu Yonadabu
mwana wa Rekabu, alitupa agizo hili:
'Ninyi wala wazao wenu kamwe msinywe
divai. 7 [m]Pia msijenge nyumba kamwe, wala
kuotesha mbegu au kupanda mashamba ya
mizabibu. Kamwe msiwe na kitu chochote
katika hivi, lakini siku zote lazima muishi
kwenye mahema. Ndipo mtakapoishi
kwa muda mrefu katika nchi ambayo
ninyi ni wahamiaji.' 8 [n]Tumetii kila kitu
ambacho baba yetu Yonadabu mwana wa
Rekabu alituamuru. Sisi wenyewe wala
wake zetu wala wana wetu na binti zetu
kamwe hatujanywa divai 9 [o]wala kujenga
nyumba za kuishi au kuwa na mashamba ya

---

[a]**34:15** Yer 7:10-11; 32:34; Neh 10:29
[b]**34:16** Eze 3:20; 18:24; Kut 20:7; Law 19:12
[c]**34:17** Mt 7:2; Gal 6:7; Yer 15:4; Kum 28:25, 64; Yer 21:7; 14:12; 29:18; 24:9
[d]**34:18** Mwa 15:10; Rum 2:8; Yer 11:10
[e]**34:19** Yer 26:10; Sef 3:3-4
[f]**34:20** Eze 16:27; 23:28; Yer 11:21; 7:33; 21:7; Kum 28:25, 64
[g]**34:21** Yer 32:4; 52:24-27; 37:5; 39:6; 2Fal 25:21
[h]**34:22** Yer 39:1-2; 37:8; 38:18; Neh 2:17; Mik 7:13; Eze 23:47
[i]**35:1** Yer 22:18; 2Nya 36:5
[j]**35:2** 2Fal 10:15; 1Nya 2:55; 1Fal 6:5; Kum 15:12
[k]**35:4** Kum 33:1; 1Nya 9:19; 2Fal 12:9; 23:4
[l]**35:6** Hes 6:2-4; Lk 1:15; Yer 35:2; 2Fal 10:15; Law 10:9
[m]**35:7** Ebr 11:9; Kut 20:12; Efe 6:2-3; Kum 4:40
[n]**35:8** Kol 3:20; Mit 1:8
[o]**35:9** 1Tim 6:6

mizabibu, mashamba au mazao. 10 Tumeishi
katika mahema na tumetii kikamilifu kila
kitu alichotuamuru baba yetu Yonadabu.
11 [a]Lakini wakati Nebukadneza mfalme
wa Babeli alipoivamia nchi hii, tulisema,
'Njooni, lazima twende Yerusalemu ili
kukimbia majeshi ya Wakaldayo na ya
Washamu.' Kwa hiyo tumeishi Yerusalemu."

12 Ndipo neno la BWANA likamjia
Yeremia kusema: 13 [b]"Hili ndilo BWANA
Mwenye Nguvu Zote, aliye Mungu wa
Israeli, asemalo: Nenda ukawaambie
watu wa Yuda na watu wa Yerusalemu,
'Je, hamwezi kujifunza kutoka kwa wana
wa Rekabu, na kuyatii maneno yangu?'
asema BWANA. 14 [c]"Yonadabu mwana wa
Rekabu aliwaagiza wanawe wasinywe
divai, na agizo hilo wamelishika mpaka leo
hawanywi divai, kwa sababu wanatii amri
ya baba yao. Lakini nimenena nanyi tena
na tena, lakini hamkunitii mimi. 15 [d]Tena na
tena nimewatuma watumishi wangu wote
manabii kwenu. Wakasema, "Kila mmoja
wenu ni lazima ageuke na kuacha njia zake
mbaya, na kuyatengeneza matendo yake.
Msifuate miungu mingine ili kuitumikia.
Ndipo mtakapoishi katika nchi niliyowapa
ninyi na baba zenu." Lakini hamkujali wala
kunisikiliza. 16 [e]Wazao wa Yonadabu mwana
wa Rekabu walitimiza amri ambayo baba
yao aliwapa, lakini watu hawa hawakunitii
mimi.'

17 [f]"Kwa hiyo, hili ndilo BWANA Mungu
Mwenye Nguvu Zote, Mungu wa Israeli,
asemalo: 'Sikilizeni! Nitaleta juu ya Yuda
na juu ya kila mmoja aishiye Yerusalemu
kila aina ya maafa niliyotamka dhidi
yao. Nilinena nao, lakini hawakusikiliza.
Niliwaita, lakini hawakujibu.' "

18 [g]Kisha Yeremia akaiambia jamaa ya
Warekabi, "Hili ndilo asemalo BWANA
Mwenye Nguvu Zote, Mungu wa Israeli:
'Mmetii amri ya baba yenu Yonadabu,
na mmefuata mafundisho yake yote na
mmefanya kila kitu alichowaamuru.'
19 [h]Kwa hiyo hili ndilo BWANA Mwenye
Nguvu Zote, Mungu wa Israeli, asemalo:
'Yonadabu mwana wa Rekabu hatakosa
kamwe kuwa na mtu wa kunitumikia
mimi.' "

*Yehoyakimu Achoma Kitabu Cha Yeremia*

36 [i]Katika mwaka wa nne wa Yehoyakimu
mwana wa Yosia mfalme wa Yuda,
neno hili lilimjia nabii Yeremia kutoka kwa
BWANA, kusema: 2 [j]"Chukua kitabu uandike
ndani yake maneno yote niliyonena nawe
kuhusu Israeli, Yuda na mataifa mengine
yote, tangu nilipoanza kunena nawe wakati
wa utawala wa Yosia hadi sasa. 3 [k]Labda
watu wa Yuda watakaposikia juu ya kila
maafa ninayokusudia kuwapiga nayo, kila
mmoja wao atageuka kutoka njia zake
mbaya, kisha nitasamehe uovu wao na
dhambi yao."

4 [l]Hivyo Yeremia akamwita Baruku
mwana wa Neria, naye Yeremia alipokuwa
akiyakariri maneno yote aliyoyasema
BWANA, Baruku akayaandika katika kitabu.
5 Kisha Yeremia akamwambia Baruku,
"Nimezuiliwa, mimi siwezi kuingia katika
Hekalu la BWANA. 6 [m]Basi wewe nenda
katika nyumba ya BWANA siku ya kufunga,
uwasomee watu maneno ya BWANA kutoka
kitabu hiki yale uliyoyaandika kutoka
kinywani mwangu. Wasomee watu wote
wa Yuda waliofika kutoka miji yao. 7 [n]Labda
wataomba na kusihi mbele za BWANA na
kila mmoja akageuka kutoka njia zake
mbaya, kwa sababu hasira na ghadhabu

[a]**35:11** 2Fal 24:1; Yer 8:14; Yos 10:20
[b]**35:13** Yer 6:10; 32:33; 11:6
[c]**35:14** Yer 7:13; 25:3; Isa 30:9
[d]**35:15** Yer 7:25; 26:3; 6:10; 25:5; 7:25; 2Fal 17:13; Eze 14:6; Isa 59:20
[e]**35:16** Law 20:9; Mal 1:6
[f]**35:17** Yos 23:15; 1Fal 13:34; Mit 1:24; Rum 10:21; Isa 66:4; 65:12; Yer 21:4-7
[g]**35:18** Mwa 31:35
[h]**35:19** Isa 48:19; Yer 33:17; 15:19
[i]**36:1** 2Nya 36:5
[j]**36:2** Yer 25:3; Za 40:7; Hab 2:2; Kut 17:14; Eze 2:7; 25:3
[k]**36:3** Eze 12:3; Amo 5:15; Isa 6:9; Yer 18:8; Mdo 3:19; Yn 3:8; Mk 14:8; Mdo 26:20; Mk 4:12; 2Fal 17:13
[l]**36:4** Yer 32:12; Zek 5:1; Yer 45; 1; Eze 2:9; Yer 51:59
[m]**36:6** Kut 4:16; 2Nya 20:4
[n]**36:7** Yer 26:3; Kum 31:17; 29:18; Yer 37:20

zilizotamkwa dhidi ya watu hawa na
BWANA ni kubwa."
8 Baruku mwana wa Neria akafanya
kila kitu nabii Yeremia alichomwambia
kufanya. Alisoma maneno ya BWANA
katika Hekalu la BWANA kutoka kile
kitabu. 9 [a]Katika mwezi wa tisa, mnamo
mwaka wa tano wa Yehoyakimu mwana
wa Yosia mfalme wa Yuda, wakati wa
kufunga mbele za BWANA, ilitangazwa kwa
watu wote walioko Yerusalemu, na wale
wote waliokuwa wamekuja kutoka miji
ya Yuda. 10 [b]Kutoka chumba cha Gemaria
mwana wa Shafani mwandishi, kilichokuwa
katika ua wa juu kwenye ingilio la Lango
Jipya la Hekalu, Baruku akawasomea watu
wote waliokuwa katika Hekalu la BWANA
maneno ya Yeremia kutoka kwenye kile
kitabu.
11 Basi Mikaya mwana wa Gemaria,
mwana wa Shafani, aliposikia maneno
yote ya BWANA kutoka kwenye kile
kitabu, 12 [c]alishuka hadi kwenye chumba
cha mwandishi kwenye jumba la kifalme,
mahali walipokuwa wameketi maafisa wote:
yaani Elishama mwandishi, Delaya mwana
wa Shemaya, Elnathani mwana wa Akbori,
Gemaria mwana wa Shafani, Sedekia
mwana wa Hanania, na maafisa wengine
wote. 13 Baada ya Mikaya kuwaambia kila
kitu ambacho alikuwa amesikia Baruku
akiwasomea watu kutoka kwenye kile
kitabu, 14 maafisa wote wakamtuma Yehudi
mwana wa Nethania, mwana wa Shelemia,
mwana wa Kushi, kumwambia Baruku,
"Leta hicho kitabu ambacho umewasomea
watu, nawe mwenyewe uje." Ndipo
Baruku mwana wa Neria akawaendea
akiwa na hicho kitabu mkononi mwake.
15 Wakamwambia, "Tafadhali, keti na
utusomee hicho kitabu."
Ndipo Baruku akawasomea kile kitabu.
16 Walipoyasikia maneno hayo yote,
wakatazamana wao kwa wao kwa woga
na kumwambia Baruku, "Lazima tutoe
taarifa ya maneno haya yote kwa mfalme."

[a]**36:9** 2Nya 20:3; Amu 20:26
[b]**36:10** Yer 52:25; Mwa 23:10; Yer 26:10; 29:3; 26:24
[c]**36:12** Yer 26:22; 2Sam 8:17; Yer 38:4

17 Kisha wakamuuliza Baruku, "Tuambie,
uliandikaje haya yote? Je, yalitoka kinywani
mwa Yeremia?"
18 [d]Baruku akajibu, "Ndiyo, maneno haya
yote yalitoka kinywani mwa Yeremia, nami
nikayaandika kwa wino katika hiki kitabu."
19 [e]Ndipo wale maafisa wakamwambia
Baruku, "Wewe na Yeremia nendeni
mkajifiche. Mtu yeyote asijue mahali
mlipo."
20 Baada ya kuhifadhi kile kitabu ndani
ya chumba cha Elishama mwandishi,
wakamwendea mfalme katika ua wa nje na
kumwarifu kila kitu. 21 [f]Mfalme akamtuma
Yehudi akachukue kile kitabu. Yehudi
akakileta hicho kitabu kutoka kwenye
chumba cha Elishama mwandishi, na
akakisoma mbele ya mfalme na maafisa
wakiwa wamesimama kando ya mfalme.
22 [g]Ulikuwa mwezi wa tisa, na mfalme
alikuwa ameketi chumba cha wakati wa
baridi akiota moto. 23 [h]Hata ikawa kila wakati
Yehudi alipomaliza kusoma kurasa tatu au
nne za hicho kitabu, mfalme alizikata kwa
kisu cha mwandishi na kuzitupia motoni,
hadi kitabu chote kikateketea. 24 [i]Mfalme
na watumishi wake wote waliosikia yote
yaliyosomwa hawakuonyesha hofu yoyote,
wala hawakuyararua mavazi yao. 25 [j]Hata
ingawa Elnathani, Delaya na Gemaria
walimsihi mfalme asikichome kile kitabu,
yeye hakuwasikiliza. 26 [k]Badala yake,
mfalme akamwamuru Yerameeli, mwana
wa mfalme, Seraya mwana wa Azrieli, na
Shelemia mwana wa Abdeeli kuwakamata
mwandishi Baruku na nabii Yeremia. Lakini
BWANA alikuwa amewaficha.
27 Baada ya mfalme kuchoma kile kitabu
kilichokuwa na yale maneno Baruku
aliyokuwa ameyaandika kutoka kinywani
mwa Yeremia, neno la BWANA lilimjia

[d]**36:18** Isa 8:12; Mt 10:16-32; 1Pet 3:14-15
[e]**36:19** 1Fal 17:3; Yer 26:16
[f]**36:21** 2Fal 22:10
[g]**36:22** Amo 3:15; Amu 3:20
[h]**36:23** 1Fal 22:8; 2Tim 4:3
[i]**36:24** Hes 14:6; 2Fal 22:11; Isa 36:22; Mwa 37:29
[j]**36:25** Mwa 37:26; Rum 8:34
[k]**36:26** Mt 23:34; 1Fal 17:3; Za 11:1

Yeremia likisema: [28] “Chukua kitabu
kingine na uandike juu yake maneno yote
yaliyokuwa katika kile kitabu cha kwanza,
ambacho Yehoyakimu mfalme wa Yuda
amekiteketeza kwa moto. [29] [a]Mwambie pia
Yehoyakimu mfalme wa Yuda, ‘Hili ndilo
asemalo BWANA: Ulikiteketeza kile kitabu
ukasema, “Kwa nini uliandika kwenye
kitabu kwamba kwa hakika mfalme wa
Babeli angekuja na kuangamiza nchi hii,
na kuwakatilia mbali watu na wanyama
kutoka humo?” [30] [b]Kwa hiyo, hili ndilo
asemalo BWANA kuhusu Yehoyakimu
mfalme wa Yuda: Hatakuwa na mtu yeyote
atakayekalia kiti cha enzi cha Daudi; maiti
yake itatupwa nje kwenye joto wakati wa
mchana na kupigwa na baridi wakati wa
usiku. [31] [c]Nitamwadhibu yeye, watoto wake
na watumishi wake kwa ajili ya uovu wao.
Nitaleta juu yao na wote waishio Yerusalemu
na watu wa Yuda kila maafa niliyoyasema
dhidi yao, kwa sababu hawajasikiliza.’ ”

[32] [d]Kisha Yeremia akachukua kitabu
kingine na kumpa mwandishi Baruku mwana
wa Neria, naye kama Yeremia alivyosema,
Baruku akaandika juu yake maneno yote ya
kile kitabu ambacho Yehoyakimu mfalme
wa Yuda alikuwa amekichoma moto, na
maneno mengine mengi yaliyofanana na
hayo yaliyoongezewa humo.

### *Yeremia Gerezani*

37 [e]Sedekia mwana wa Yosia akafanywa
kuwa mfalme wa Yuda na Nebukadneza
mfalme wa Babeli, naye akatawala mahali
pa Yehoyakini[f] mwana wa Yehoyakimu.
[2] [g]Lakini sio Sedekia, wala watumishi wake,
wala watu wa nchi walisikiliza maneno
ya BWANA aliyonena kupitia kwa nabii
Yeremia.

[3] [h]Hata hivyo, Mfalme Sedekia akamtuma
Yehukali mwana wa Shelemia, pamoja na
kuhani Sefania mwana wa Maaseya kwa
nabii Yeremia na ujumbe huu: “Tafadhali
utuombee kwa BWANA, Mungu wetu.”

[4] [i]Wakati huu Yeremia alikuwa huru
kuingia na kutoka katikati ya watu, kwa
sababu alikuwa bado hajatiwa gerezani.
[5] [j]Jeshi la Farao lilikuwa limetoka Misri,
nao Wakaldayo waliokuwa wameuzunguka
Yerusalemu kwa majeshi waliposikia taarifa
kuhusu jeshi hilo walijiondoa Yerusalemu.

[6] Ndipo neno la BWANA likamjia nabii
Yeremia kusema: [7] [k]“Hili ndilo asemalo
BWANA, Mungu wa Israeli: Mwambie
mfalme wa Yuda aliyekutuma uniulize mimi,
‘Jeshi la Farao lililotoka kuja kukusaidia
litarudi katika nchi yake yenyewe, yaani
Misri. [8] [l]Kisha Wakaldayo watarudi na
kushambulia mji huu, watauteka na
kuuchoma moto.’

[9] [m]“Hili ndilo BWANA asemalo:
Msijidanganye wenyewe mkifikiri, ‘Hakika
Wakaldayo watatuacha na kwenda zao.’
Hakika hawatawaacha! [10] [n]Hata kama
mngelishinda jeshi lote la Wakaldayo
linalowashambulia ninyi, na wakawa ni
watu waliojeruhiwa tu waliobaki kwenye
mahema yao, wangetoka na kuuchoma mji
huu moto.”

[11] Baada ya jeshi la Wakaldayo kujiondoa
kutoka Yerusalemu kwa sababu ya jeshi la
Farao, [12] [o]Yeremia akaanza kuondoka mjini
ili kwenda nchi ya Benyamini ili akapate
sehemu yake ya milki miongoni mwa watu
huko. [13] [p]Lakini alipofika kwenye Lango la

---

[a]**36:29** Isa 30:10; Amo 5:10; Yer 33:12
[b]**36:30** Isa 14:19; Yer 22:19; 52:2; 8:2; 2Fal 24:6
[c]**36:31** Kut 20:5; Mit 29:1; 1:24
[d]**36:32** Kut 34:1; Yer 30:2; Kut 4:15; Rum 16:22
[e]**37:1** 2Fal 14:17; 1Nya 3:16; Eze 17:13; 2Nya 36:10; 24:8, 12; Yer 22:24
[f]1 Yehoyakini ni jina jingine la Yekonia au Konia.
[g]**37:2** 2Fal 24:19; 2Nya 36:12-14; Mit 29:12
[h]**37:3** 2Fal 25:18; Yer 52:24; Hes 21:7; 1Sam 12:19; Yer 38:14; Kut 8:28; 1Fal 13:6
[i]**37:4** Yer 32:2
[j]**37:5** Mwa 15; 18; Yer 34:21; 31:1; Isa 30:5; 2Fal 24:7; Eze 17:15
[k]**37:7** Mwa 25:22; 2Fal 22:18; 18:21; Yer 2:12; 36; Mao 4:17
[l]**37:8** Yer 21:10; 39; 8; Mit 21:30; Yer 38:3, 8
[m]**37:9** Yer 29:8; Mk 13:5
[n]**37:10** Law 26:36-38; Isa 30:17; Yer 21:4-5, 10
[o]**37:12** Yer 32:9
[p]**37:13** Yer 20:2; 21:9

Benyamini, mkuu wa walinzi, ambaye jina lake lilikuwa Iriya mwana wa Shelemia mwana wa Hanania, akamkamata Yeremia na kusema, “Wewe unakwenda kujiunga na Wakaldayo!”

14 [a]Yeremia akasema, “Hiyo si kweli, mimi sijiungi na Wakaldayo.” Lakini Iriya hakumsikiliza; badala yake, akamkamata Yeremia na kumpeleka kwa maafisa. 15 [b]Wakamkasirikia Yeremia, wakaamuru apigwe, na akafungwa katika nyumba ya Yonathani mwandishi waliyokuwa wameifanya gereza.

16 Yeremia akawekwa kwenye chumba kilichofukuliwa chini, kilichojengwa kwa zege ndani ya gereza chini ya ngome, akakaa huko kwa muda mrefu. 17 [c]Kisha Mfalme Sedekia akatumana aletwe katika jumba la kifalme, mahali alipomuuliza kwa siri, “Je, kuna neno lolote kutoka kwa Bwana?”

Yeremia akajibu, “Ndiyo, utatiwa mikononi mwa mfalme wa Babeli.”

18 [d]Kisha Yeremia akamwambia Mfalme Sedekia, “Nimefanya kosa gani dhidi yako na maafisa wako au watu hawa, hata ukanitia gerezani? 19 [e]Wako wapi manabii wako waliokutabiria wakisema, ‘Mfalme wa Babeli hatakushambulia wewe wala nchi hii?’ 20 Lakini sasa, bwana wangu mfalme, tafadhali sikiliza. Niruhusu nilete maombi yangu mbele yako, usinirudishe kwenye nyumba ya Yonathani mwandishi, nisije nikafia humo.”

21 [f]Ndipo Mfalme Sedekia akatoa maagizo Yeremia awekwe katika ua wa walinzi, na apewe mkate kutoka mitaa ya waokaji kila siku mpaka mikate yote katika mji itakapokwisha. Kwa hiyo Yeremia akabaki katika ua wa walinzi.

[a]**37:14** Isa 58:6; Yer 40:4
[b]**37:15** Yer 20:2; 38:26; Ebr 11:36; Mdo 5:40; 12:6; 1Fal 22:27
[c]**37:17** Yer 15:11; 38:16; 21:7; Mwa 25:22
[d]**37:18** 1Sam 16:18; Yn 10:32; Mdo 25:8
[e]**37:19** Yer 14:13; Eze 13:2
[f]**37:21** Law 26:26; 2Kor 4; 6; Isa 33:16; 2Fal 25:3; Yer 52:6; 39:13-14

### *Yeremia Atupwa Kwenye Kisima*

38 [g]Shefatia mwana wa Matani, na Gedalia mwana wa Pashuri, na Yehukali mwana wa Shelemia, na Pashuri mwana wa Malkiya wakasikia kile Yeremia alichokuwa akiwaambia watu wote wakati aliposema, 2 [h]“Hili ndilo asemalo Bwana: ‘Yeyote akaaye ndani ya mji huu atakufa kwa upanga, njaa au tauni, lakini yeyote atakayejisalimisha kwa Wakaldayo ataishi. Atakayeyatoa maisha yake kama nyara, ataishi.’ 3 [i]Tena hili ndilo asemalo Bwana: ‘Mji huu kwa hakika utatiwa mikononi mwa jeshi la mfalme wa Babeli, ambaye atauteka.’ ”

4 [j]Ndipo maafisa wakamwambia mfalme, “Mtu huyu imempasa kuuawa. Anawakatisha tamaa askari waliobaki katika mji huu, vivyo hivyo na watu wote pia, kwa ajili ya mambo anayowaambia. Mtu huyu hawatakii mema watu hawa, bali maangamizi yao.”

5 [k]Mfalme Sedekia akajibu, “Yeye yuko mikononi mwenu! Mfalme hawezi kufanya lolote kuwapinga ninyi.”

6 [l]Basi wakamchukua Yeremia na kumtia kwenye kisima cha Malkiya, mwana wa mfalme, kilichokuwa katika ua wa walinzi. Wakamteremsha Yeremia kwa kamba ndani ya kisima. Hakikuwa na maji ndani yake, ila tope tu, naye Yeremia akazama ndani ya matope.

7 [m]Lakini Ebed-Meleki Mkushi, aliyekuwa afisa katika jumba la kifalme, akasikia kuwa walikuwa wamemtia Yeremia ndani ya kisima. Wakati mfalme alipokuwa ameketi katika Lango la Benyamini, 8 Ebed-Meleki akatoka nje ya jumba la kifalme na kumwambia, 9 [n]“Mfalme bwana wangu,

[g]**38:1** Yer 37:3; Mdo 4:2; 1Nya 9:12
[h]**38:2** Yer 34:17; 11:21; 45:5; 21:9; 38:19; Mt 24:7-8
[i]**38:3** Yer 21:10; 32:3
[j]**38:4** Yer 36:12; 11:21; 26:11; Za 37:12-40; Amo 7:10; 1Sam 17:32
[k]**38:5** Yer 26:14; 1Sam 15:24
[l]**38:6** Yer 37:21; Mao 3:53; Mk 9:42; Yos 2:15; Mwa 37:24; Ay 30:9
[m]**38:7** Yer 39:16; Isa 56:3-5; Mdo 8:27; Ay 29:7
[n]**38:9** Yer 37:21; Mwa 37:20

watu hawa wamefanya uovu kwa yote
waliomtendea nabii Yeremia. Wamemtupa
ndani ya kisima, mahali ambapo atakufa
kwa njaa wakati ambapo hakuna chakula
popote katika mji."
10 Basi mfalme akamwamuru Ebed-Meleki
Mkushi, akisema, "Chukua watu thelathini
kutoka hapa pamoja nawe, mkamtoe nabii
Yeremia huko kwenye kisima kabla hajafa."
11 Basi Ebed-Meleki akawachukua watu
pamoja naye, wakaenda mpaka kwenye
chumba kilichoko chini ya hazina ndani
ya jumba la kifalme. Akachukua matambaa
makuukuu pamoja na nguo zilizochakaa
kutoka huko, na kumshushia Yeremia kwa
kamba ndani ya kisima. 12 Ebed-Meleki
Mkushi akamwambia Yeremia, "Weka
haya matambaa makuukuu na hizo nguo
zilizochakaa makwapani ili kuzuia kamba."
Yeremia akafanya hivyo, 13 [a]nao wakamvuta
juu kwa kamba na kumtoa katika kisima.
Yeremia akakaa katika ua wa walinzi.

*Sedekia Amhoji Yeremia Tena*

14 [b]Ndipo Mfalme Sedekia akatuma watu
wamwitie nabii Yeremia wamlete kwake
kwenye ingilio la tatu la Hekalu la BWANA.
Mfalme akamwambia Yeremia, "Ninataka
kukuuliza jambo fulani, usinifiche kitu
chochote."
15 Yeremia akamwambia Sedekia,
"Nikikupa jibu, je, hutaniua? Hata kama
nikikupa shauri, wewe hutanisikiliza."
16 [c]Lakini Mfalme Sedekia akamwapia
Yeremia kiapo hiki kwa siri, akisema,
"Hakika kama aishivyo BWANA, ambaye
ametupa pumzi, sitakuua wala sitakutia
mikononi mwa wale wanaotafuta uhai
wako."
17 [d]Kisha Yeremia akamwambia Sedekia,
"Hili ndilo asemalo BWANA Mungu Mwenye
Nguvu Zote, Mungu wa Israeli: 'Ikiwa
utajisalimisha kwa maafisa wa mfalme wa
Babeli, maisha yako yatasalimika, na mji
huu hautateketezwa kwa moto. Pia wewe
na jamaa yako mtaishi. 18 [e]Lakini ikiwa
hutajisalimisha kwa maafisa wa mfalme
wa Babeli, mji huu utatiwa mikononi mwa
Wakaldayo na watauteketeza kwa moto,
nawe mwenyewe hutaweza kujiokoa
mikononi mwao.' "
19 [f]Mfalme Sedekia akamwambia
Yeremia, "Ninawaogopa Wayahudi ambao
wamekimbilia kwa Wakaldayo, kwa kuwa
Wakaldayo wanaweza kunitia mikononi
mwao, nao wakanitenda vibaya."
20 [g]Yeremia akajibu, "Hawatakutia
mikononi mwao. Mtii BWANA kwa kufanya
kile ninachokuambia. Kisha utafanikiwa
na maisha yako yatakuwa salama.
21 Lakini ukikataa kujisalimisha, hili ndilo
BWANA alilonifunulia: 22 [h]Wanawake
wote walioachwa katika jumba la kifalme
la mfalme wa Yuda wataletwa mbele ya
maafisa wa mfalme wa Babeli. Wanawake
hao watakuambia:

" 'Walikupotosha na kukushinda,
  wale rafiki zako uliowaamini.
Miguu yako imezama matopeni;
  rafiki zako wamekuacha.'

23 [i]"Wake zako wote na watoto wataletwa
na kutiwa mikononi mwa Wakaldayo.
Wewe mwenyewe hutaweza kujiokoa
mikononi mwao. Lakini utatekwa na
mfalme wa Babeli, na mji huu utateketezwa
kwa moto."
24 [j]Kisha Sedekia akamwambia Yeremia,
"Usiruhusu mtu yeyote ajue kuhusu haya
mazungumzo, la sivyo utakufa. 25 Maafisa
wakisikia kwamba nimezungumza nawe,
nao wakakujia na kusema, 'Tuambie
kile ulichozungumza na mfalme na kile
mfalme alichokuambia, usitufiche au sivyo
tutakuua,' 26 [k]basi waambie, 'Nilikuwa

[a]**38:13** Yer 37:21; 2Kor 6:4-5
[b]**38:14** 1Sam 3:17; Za 82:4; Yer 37:3
[c]**38:16** Yer 37:17; Hes 16:22; Isa 42:5; 57:16; Ebr 12:9
[d]**38:17** 2Fal 24:12; Yer 21:8-10; 27:8
[e]**38:18** Yer 34:3; 37:8; 24:8; 32:4
[f]**38:19** Isa 51:12; Yn 12:42; Yer 52:15; 1Sam 31:4; Yer 39:9
[g]**38:20** Yer 11:4; Isa 55:3; 2Kor 5:20; Kum 5:33; Yer 40:9
[h]**38:22** Yer 6:12; Ay 19:14; Yer 13:21; Ay 30:19; Za 69:14
[i]**38:23** 2Fal 25:6; Yer 24:8; 41:10; 32:4; Eze 17:15; Yer 21:10; 37:8
[j]**38:24** Yer 37:17-21
[k]**38:26** Yer 37:15, 20; 39:14; 1Sam 16:2

ninamsihi mfalme asinirudishe kwenye
nyumba ya Yonathani nisije nikafia humo.' "
27 Maafisa wote wakamjia Yeremia na
kumuuliza, naye Yeremia akawaambia
kila kitu mfalme alichomwagiza kusema.
Kisha hawakusema lolote zaidi na Yeremia
kwa sababu hakuna yeyote aliyesikia
mazungumzo yake na mfalme.
28 Naye Yeremia akabaki katika ua wa
walinzi hadi siku Yerusalemu ilipotekwa.

*Anguko La Yerusalemu*

39 [a]Hivi ndivyo Yerusalemu ilivyotwaliwa:
Katika mwaka wa tisa wa utawala wa
Mfalme Sedekia wa Yuda, katika mwezi
wa kumi, Nebukadneza mfalme wa Babeli
akiwa na jeshi lake lote alifanya vita
dhidi ya Yerusalemu na akauzunguka mji.
2 [b]Katika siku ya tisa ya mwezi wa nne
wa mwaka wa kumi na moja wa utawala
wa Sedekia, ukuta wa mji ulibomolewa.
3 [c]Kisha maafisa wote wa mfalme wa Babeli
wakaja na kuketi kwenye Lango la Kati,
nao ni: Nergal-Shareza wa Samgari, Nebo-
Sarsekimu afisa mkuu, Nergal-Shareza
afisa mwenye cheo cha juu, na maafisa
wengine wote wa mfalme wa Babeli.
4 [d]Mfalme Sedekia wa Yuda na askari wote
walipowaona, wakakimbia na kuondoka
mjini usiku kwa njia ya bustani ya mfalme,
kupitia lango lililokuwa kati ya kuta mbili,
wakaelekea Araba.[e]
5 [f]Lakini jeshi la Wakaldayo likawafuatia
na kumpata Sedekia katika sehemu
tambarare za Yeriko. Wakamkamata na
kumpeleka kwa Nebukadneza mfalme wa
Babeli huko Ribla, katika nchi ya Hamathi,
mahali ambapo alimtangazia hukumu.
6 Huko Ribla, mfalme wa Babeli aliwachinja
wana wa Sedekia mbele ya macho yake, na
pia akawaua wakuu wote wa Yuda. 7 [g]Kisha
akayang'oa macho ya Sedekia na kumfunga
kwa pingu za shaba na kumpeleka Babeli.
8 [h]Jeshi la Wakaldayo likachoma moto
jumba la kifalme na nyumba za watu,
na kuzibomoa kuta za Yerusalemu.
9 [i]Nebuzaradani kiongozi wa walinzi wa
mfalme akawachukua na kuwapeleka
uhamishoni Babeli watu waliokuwa
wamebaki ndani ya mji, pamoja na wale
waliokuwa wamejisalimisha kwake, na
watu wengine wote. 10 Lakini Nebuzaradani
kiongozi wa walinzi aliwabakiza baadhi
ya watu maskini katika nchi ya Yuda,
ambao hawakuwa na kitu. Naye wakati
huo akawapa mashamba ya mizabibu na
mashamba mengine.
11 Basi, Nebukadneza mfalme wa Babeli
alikuwa ametoa maagizo kuhusu Yeremia
kupitia Nebuzaradani kiongozi wa walinzi
wa mfalme akisema: 12 [j]"Mchukue umtunze.
Usimdhuru, lakini umfanyie chochote
anachotaka." 13 Basi Nebuzaradani kiongozi
wa walinzi, Nebushazbani afisa mkuu,
Nergal-Shareza afisa wa cheo cha juu, na
maafisa wengine wote wa mfalme wa Babeli
14 [k]wakatuma watu kumwondoa Yeremia
kutoka ua wa walinzi. Wakamkabidhi kwa
Gedalia mwana wa Ahikamu mwana wa
Shafani, ili amrudishe nyumbani kwake.
Kwa hiyo akabaki miongoni mwa watu
wake mwenyewe.
15 Wakati Yeremia alipokuwa amezuiliwa
katika ua wa walinzi, neno la BWANA
lilimjia kusema: 16 [l]"Nenda ukamwambie
Ebed-Meleki Mkushi, 'Hili ndilo BWANA
Mwenye Nguvu Zote, Mungu wa Israeli,
asemalo: Ninakaribia kutimiza maneno
yangu dhidi ya mji huu kwa njia ya maafa,
wala si kwa kuwafanikisha. Wakati huo
hayo yatatimizwa mbele ya macho yako.
17 [m]Lakini siku hiyo nitakuokoa, asema

---

[a]**39:1** 2Fal 25:1; Eze 4:3; Yer 52:4-7; 25:29; 2Nya 36:11; Yer 28:14; Eze 24:2
[b]**39:2** Zek 8:19; 2Fal 14:13; Eze 33:21
[c]**39:3** Yer 21:4
[d]**39:4** Eze 12:12; Isa 22:11
[e]4 Au: kuelekea Bonde la Yordani.
[f]**39:5** Yer 24:8; Hes 34:11; 2Fal 23:33; Yos 5:10; Yer 34:18; 32:4
[g]**39:7** Hes 16:14; Eze 12:13; Yer 2:35
[h]**39:8** Yer 34:22; 38:18; Za 80:12; Mao 2:8; Isa 22:5
[i]**39:9** Yer 40:1; Mao 1:5; Yer 52:15; 21:9
[j]**39:12** Mit 16:7; 1Pet 3:13; Yer 15:20-21
[k]**39:14** Neh 3:25; Yer 38:28; 2Fal 22:12; Yer 40:5; 37:21
[l]**39:16** Yer 38:7; Yos 23:15; Dan 9:12; Za 33:11; Isa 14:27; 40:8; Mao 2:17; Yer 44:28
[m]**39:17** Za 34:22; 41:1-2

BWANA; hutatiwa mikononi mwa wale
unaowaogopa. 18 [a]Nitakuokoa; hutaanguka
kwa upanga, lakini maisha yako yatakuwa
salama, kwa sababu unanitumaini, asema
BWANA.' ”

*Yeremia Aachiwa Huru*

40 [b]Neno likamjia Yeremia kutoka kwa
BWANA baada ya Nebuzaradani
kiongozi wa walinzi wa mfalme kumfungua
huko Rama. Alikuwa amemkuta Yeremia
akiwa amefungwa kwa minyororo miongoni
mwa mateka wote kutoka Yerusalemu na
Yuda waliokuwa wakipelekwa uhamishoni
Babeli. 2 [c]Kiongozi wa walinzi alipomwona
Yeremia, akamwambia, “BWANA Mungu
wako aliamuru maafa haya kwa mahali
hapa. 3 [d]Sasa BWANA ameyaleta haya,
amefanya sawasawa na vile alivyosema
angefanya. Yote haya yametokea kwa
sababu ninyi mlifanya dhambi dhidi
ya BWANA na hamkumtii. 4 [e]Lakini leo
ninakufungua minyororo iliyo kwenye
viwiko vya mikono yako. Twende pamoja
mpaka Babeli ikiwa unataka, nami
nitakutunza. Lakini kama hutaki, basi usije.
Tazama, nchi yote iko mbele yako, nenda
kokote unakotaka.” 5 [f]Lakini kabla Yeremia
hajageuka kuondoka, Nebuzaradani
akaongeza kusema, “Rudi kwa Gedalia
mwana wa Ahikamu mwana wa Shafani,
ambaye mfalme wa Babeli amemchagua
awe juu ya miji ya Yuda, ukaishi naye
miongoni mwa watu, au uende popote
panapokupendeza.”

Kisha huyo kiongozi akampa posho yake
na zawadi, akamwacha aende zake. 6 [g]Kwa
hiyo Yeremia akaenda kwa Gedalia mwana
wa Ahikamu huko Mispa, na kuishi naye
miongoni mwa watu walioachwa katika
nchi.

*Gedalia Auawa*

**(2 Wafalme 25:22-26)**

7 [h]Maafisa wote wa jeshi na watu wao
waliokuwa bado wapo kwenye eneo la wazi
waliposikia kwamba mfalme wa Babeli
amemteua Gedalia mwana wa Ahikamu
kuwa mtawala wa nchi, na amemweka
kuwa kiongozi wa wanaume, wanawake
na watoto waliokuwa maskini zaidi katika
nchi ambao hawakuchukuliwa kwenda
uhamishoni Babeli, 8 [i]wakamjia Gedalia
huko Mispa. Hawa walikuwa Ishmaeli
mwana wa Nethania, Yohanani na
Yonathani wana wa Karea, Seraya mwana
wa Tanhumethi, wana wa Efai Mnetofathi,
na Yezania mwana wa Mmaaka, pamoja na
watu wao. 9 [j]Gedalia mwana wa Ahikamu
mwana wa Shafani akaapa ili kuwatia moyo
wao na watu wao. Akasema: “Msiogope
kuwatumikia Wakaldayo. Kaeni katika
nchi na kumtumikia mfalme wa Babeli, na
itakuwa vyema kwenu. 10 [k]Mimi mwenyewe
nitakaa Mispa ili kuwawakilisha mbele
ya Wakaldayo wanaotujia, lakini ninyi
mtavuna divai, matunda ya kiangazi na
mafuta, nanyi mtaweka katika vyombo
vyenu vya kuhifadhia, na kuishi katika miji
mliyojitwalia.”

11 [l]Wayahudi wote waliokuwa Moabu,
Amoni, Edomu na nchi nyingine zote
waliposikia kwamba mfalme wa Babeli
ameacha mabaki ya watu katika Yuda na
amemweka Gedalia mwana wa Ahikamu
mwana wa Shafani kuwa mtawala wao,

[a]**39:18** Ay 5:20; Yer 45:5; 21:9; 38:2; Rum 10:11; Rut 2:12; 1Nya 5:20; 1Sam 17:47; Mdo 16:31
[b]**40:1** Yer 39:14; Mt 2:18; Yos 18:25; Nah 3:10; 1Sam 8:4
[c]**40:2** Yos 23:15; Yer 50:7; Mao 2:17; Rum 13:4; Isa 10:22; 2Nya 34:24; Za 18:18; Gal 6:7-8
[d]**40:3** Mit 13:21; Yak 1:15; Law 26:33; Mdo 7:39; Rum 6:23; Kum 29:24-28; Dan 9:14; Rum 2:5-9
[e]**40:4** Mwa 13:9; Yer 39:11-12; Mwa 20:15; Za 105:18-20; Yer 37:14; Mao 3:7
[f]**40:5** 2Fal 25:22; Yer 39:14; Yos 15:18; Mit 15:16; 2Fal 22:12-14; Neh 5:14; Zek 1:12
[g]**40:6** Amu 20:1; 1Sam 7:5-17
[h]**40:7** Yer 39:10; Mdo 24:17; Mwa 41:41; Neh 5:14; Yak 2:5; 2Fal 24:14
[i]**40:8** Yer 41:1-2; 2Sam 23:28; Kum 3:14
[j]**40:9** Yer 5:19; Efe 6:5-8; Yer 38:20; Rum 13:1-2; Eze 23:23
[k]**40:10** Kum 1:39; 16:13; Mwa 27:28; Kut 7:19; 23:16; 2Kor 4:7
[l]**40:11** Hes 21:11; 25:1; Isa 16:4; Mao 1:14; Yer 24:9; Mwa 25:30; Yer 12:14

12 [a]wakarudi wote katika nchi ya Yuda
kwa Gedalia huko Mispa, kutoka nchi zote
ambazo walikuwa wametawanywa. Nao
wakavuna divai na matunda tele wakati
wa kiangazi.
13 Yohanani mwana wa Karea pamoja
na maafisa wote wa jeshi waliokuwa bado
wapo kwenye eneo la wazi wakamjia
Gedalia huko Mispa 14 [b]na kumwambia,
“Je, hujui kwamba Baalisi mfalme wa
Waamoni amemtuma Ishmaeli mwana wa
Nethania akuue?” Lakini Gedalia mwana
wa Ahikamu hakuwaamini.
15 [c]Kisha Yohanani mwana wa Karea
akamwambia Gedalia kwa siri huko Mispa,
“Acha niende nikamuue Ishmaeli mwana
wa Nethania, wala hakuna atakayejua. Kwa
nini akuue na kusababisha Wayahudi wote
waliokuzunguka watawanyike, na mabaki
wa Yuda waangamie?”
16 [d]Lakini Gedalia mwana wa Ahikamu
akamwambia Yohanani mwana wa Karea,
“Usifanye jambo kama hilo! Unalosema
kuhusu Ishmaeli si kweli.”

41 [e]Katika mwezi wa saba Ishmaeli
mwana wa Nethania mwana wa
Elishama, aliyekuwa wa uzao wa mfalme
na pia alikuwa mmoja wa maafisa wa
mfalme, akaja pamoja na watu kumi
kwa Gedalia mwana wa Ahikamu huko
Mispa. Walipokuwa wakila pamoja huko,
2 [f]Ishmaeli mwana wa Nethania pamoja na
wale watu kumi waliokuwa pamoja naye
waliinuka na kumuua Gedalia mwana wa
Ahikamu mwana wa Shafani kwa upanga,
wakamuua yule ambaye mfalme wa Babeli
alikuwa amemteua awe mtawala wa nchi.
3 Ishmaeli akawaua pia Wayahudi wote
waliokuwa na Gedalia huko Mispa, pamoja
na askari wa Kikaldayo waliokuwa huko.
4 Siku moja baada ya kuuawa kwa siri
kwa Gedalia, kabla mtu yeyote hajafahamu
jambo hilo, 5 [g]watu themanini waliokuwa
wamenyoa ndevu zao, waliorarua nguo zao
na kujikatakata walikuja kutoka Shekemu,
Shilo na Samaria wakileta sadaka za nafaka
na uvumba katika nyumba ya Bwana.
6 [h]Ishmaeli mwana wa Nethania akaondoka
Mispa ili kwenda kuwalaki, huku akilia
alipokuwa akienda. Alipokutana nao,
akasema, “Karibuni kwa Gedalia mwana
wa Ahikamu.” 7 [i]Walipoingia mjini,
Ishmaeli mwana wa Nethania na wale watu
waliokuwa pamoja naye wakawachinja na
kuwatupa ndani ya kisima. 8 [j]Lakini watu
kumi miongoni mwao wakamwambia
Ishmaeli, “Sisi usituue! Tuna ngano na
shayiri, mafuta na asali, vilivyofichwa
katika shamba.” Kwa hiyo akawaacha na
hakuwaua pamoja na wale wengine. 9 [k]Basi
kile kisima ambacho alitupa zile maiti za
watu aliowaua pamoja na Gedalia kilikuwa
ni kile kisima ambacho Mfalme Asa
alikifanya sehemu ya ulinzi wake dhidi ya
Baasha mfalme wa Israeli. Ishmaeli mwana
wa Nethania akakijaza kisima hicho kwa
maiti.
10 [l]Ishmaeli akawafanya mateka watu wote
ambao Nebuzaradani kiongozi wa walinzi
wa mfalme alikuwa amewaacha huko Mispa
na kumweka Gedalia mwana wa Ahikamu
juu yao: walikuwa binti za mfalme pamoja
na watu wote aliokuwa amewaacha huko.
Ishmaeli mwana wa Nethania akawachukua
mateka na kuondoka nao, akavuka kwenda
kwa Waamoni.
11 [m]Yohanani mwana wa Karea na maafisa
wote wa jeshi waliokuwa pamoja naye
waliposikia juu ya uhalifu wote ambao
Ishmaeli mwana wa Nethania alikuwa

[a]**40:12** Yer 43:5
[b]**40:14** Mwa 19:38; 2Sam 10:1-19; Amo 1:13; Yer 41:10; 25:21; 49:1
[c]**40:15** Kum 5:17; Mt 5:21-22; Mwa 11:4; Mt 26:31; Yn 11:52; Rum 11:5; 2Fal 21:15
[d]**40:16** Yer 43:2
[e]**41:1** Yer 40:8; Lk 22:21; Za 41:9
[f]**41:2** Za 41:9; Yer 40:5; 2Sam 3:27; Rum 3:15; Yos 11:10; Ebr 11:37; 2Sam 20:9-10; Yer 40:8
[g]**41:5** Law 19:27; Yer 48:37; Mwa 12:6; 1Fal 16:24; 3:2; Isa 15:2; Yer 47:5; Hes 16:40; Amu 9:1-57; Mk 14:63
[h]**41:6** 2Sam 5:16; Ufu 20:10; Hos 7:11; Za 5:9
[i]**41:7** Mwa 27:24; 2Fal 10:14
[j]**41:8** Isa 45:3
[k]**41:9** 1Fal 15:22; 2Nya 16:6; Amu 6:2; Yos 10:16-18
[l]**41:10** Yer 40:7, 12-14; Neh 2:10, 19
[m]**41:11** Yer 40:8-13

ameufanya, 12 [a]waliwachukua watu wao
wote kwenda kupigana na Ishmaeli mwana
wa Nethania. Wakakutana naye karibu na
bwawa kubwa huko Gibeoni. 13 Ikawa watu
wote waliokuwa na Ishmaeli walipomwona
Yohanani mwana wa Karea pamoja na
maafisa wa jeshi waliokuwa pamoja naye,
wakafurahi. 14 Watu wote ambao Ishmaeli
alikuwa amewachukua mateka huko Mispa
wakageuka na kumfuata Yohanani mwana
wa Karea. 15 [b]Lakini Ishmaeli mwana wa
Nethania pamoja na watu wake wanane
wakamtoroka Yohanani na kukimbilia kwa
Waamoni.

### *Kukimbilia Misri*

16 [c]Ndipo Yohanani mwana wa Karea
pamoja na maafisa wote wa jeshi
waliokuwa pamoja naye wakawaongoza
wote walionusurika kutoka Mispa, ambao
walipona kutoka mikononi mwa Ishmaeli
mwana wa Nethania baada yake kumuua
Gedalia mwana wa Ahikamu: walikuwa
askari, wanawake, watoto na matowashi
aliowaleta kutoka Gibeoni. 17 [d]Kisha
wakaenda mbele na kutua Geruth-Kimhamu
karibu na Bethlehemu wakiwa njiani
kwenda Misri 18 [e]ili kuwatoroka Wakaldayo.
Waliwaogopa kwa sababu Ishmaeli mwana
wa Nethania alikuwa amemuua Gedalia
mwana wa Ahikamu, ambaye alikuwa
amewekwa na mfalme wa Babeli kuwa
mtawala wa nchi.

### *Yeremia Ashauri Walionusurika Wasihame Yuda*

42 [f]Ndipo maafisa wote wa jeshi, pamoja
na Yohanani mwana wa Karea, na
Yezania mwana wa Hoshaya, na watu
wote kuanzia aliye mdogo kabisa hadi aliye
mkuu sana wakamjia 2 [g]Yeremia nabii na
kumwambia, "Tafadhali sikia maombi yetu
na umwombe BWANA Mungu wako kwa
ajili ya watu hawa wote waliosalia. Kwa
kuwa kama unavyoona sasa, ingawa wakati
fulani tulikuwa wengi, sasa tumesalia
wachache tu. 3 [h]Omba ili BWANA Mungu
wako atuambie twende wapi na tufanye
nini."

4 [i]Nabii Yeremia akajibu, "Nimewasikia.
Kwa hakika nitamwomba BWANA Mungu
wenu kama mlivyoomba. Nitawaambia kila
kitu asemacho BWANA, wala sitawaficha
chochote."

5 [j]Kisha wakamwambia Yeremia, "BWANA
na awe shahidi wa kweli na mwaminifu kati
yetu kama hatutafanya sawasawa na kila
kitu BWANA Mungu wako atakachokutuma
utuambie. 6 [k]Likiwa jema au likiwa baya,
tutamtii BWANA Mungu wetu, ambaye
tunakutuma kwake, ili mambo yote yawe
mema kwetu, kwa maana tutamtii BWANA
Mungu wetu."

7 Baada ya siku kumi, neno la BWANA
likamjia Yeremia. 8 [l]Kwa hiyo akawaita
pamoja Yohanani mwana wa Karea, na
maafisa wote wa jeshi waliokuwa pamoja
naye na watu wote kuanzia mdogo kabisa
hadi aliye mkuu sana. 9 Akawaambia,
"Hili ndilo asemalo BWANA, Mungu wa
Israeli, ambaye mlinituma kuwasilisha
maombi yenu: 10 [m]'Kama mkikaa katika
nchi hii, nitawajenga wala sitawabomoa,
nitawapanda wala sitawang'oa, kwani
ninahuzunishwa na maafa niliyowapiga
nayo. 11 [n]Msimwogope mfalme wa Babeli,

[a]**41:12** 2Sam 2:13; Yn 9:7; Kut 14:14; Yn 18:36; Yos 9:3
[b]**41:15** Yos 21:30; Mit 28; 17; 1Sam 30:17
[c]**41:16** Yer 42:1; 43:2-4; Eze 7:16; 14:22; Sef 2:9
[d]**41:17** 2Sam 19:37; Yer 42:14; Mwa 35:19; Mik 5:2
[e]**41:18** Hes 14:9; Lk 12:4-5; Yer 40:5; Isa 5:12; Yer 42:16; 2Fal 25:22
[f]**42:1** Yer 40:13; 6:13; 41:11; 44:12
[g]**42:2** Mwa 20:7; Yak 5:16; Law 26:22; Mdo 8:24; Yer 36:7
[h]**42:3** Ezr 8:21; Za 86:11; Mit 3:6; Yer 15:11
[i]**42:4** Kut 8:29; 1Sam 12:23; Hes 22:18; 1Fal 22:14; 1Sam 3:17
[j]**42:5** Kum 4:26; 1Fal 22:16; Za 119:160; Rum 3:4; Yn 8:26; Mwa 31:48; Isa 1:2; Rum 1:9; Ufu 1:5
[k]**42:6** Kum 5:29; 6:3; Yer 7:23; 43:4; Mhu 3:2; Dan 11:4; 2Nya 34:24; Eze 36:36
[l]**42:8** Ebr 8:11; Lk 7:28; Mk 9:35; Yer 4:16
[m]**42:10** Yer 24:6; Kum 30:6; Yer 31:28; 43:4; Mhu 3:2; Dan 11:4; 2Nya 34:24; Eze 36; 36
[n]**42:11** Eze 30:18; Hes 14:9; Yer 27:11; Ebr 7:25; Rum 8:31; Mit 20:22; 1Sam 15:24

ambaye sasa mnamwogopa. Msimwogope,
asema BWANA, kwa kuwa niko pamoja
nanyi, nami nitawaokoa na kuwaponya
kutoka mikononi mwake. 12 [a]Nitawaonea
huruma ili naye awe na huruma nanyi na
kuwarudisha katika nchi yenu.'

13 [b]"Hata hivyo, kama mkisema,
'Hatutakaa katika nchi hii,' hivyo mkaacha
kumtii BWANA Mungu wenu, 14 [c]nanyi kama
mkisema, 'Hapana, tutakwenda kuishi
Misri, mahali ambapo hatutaona vita au
kusikia sauti ya tarumbeta au kuwa na
njaa ya chakula,' 15 basi sikieni neno la
BWANA, enyi mabaki ya Yuda. Hili ndilo
BWANA Mwenye Nguvu Zote, Mungu
wa Israeli, asemalo: 'Ikiwa mmekusudia
kwenda Misri na kufanya makazi huko,
16 [d]basi ule upanga mnaouogopa utawapata
huko, na njaa mnayoihofia itawafuata huko
Misri, nanyi mtafia huko. 17 [e]Naam, wote
waliokusudia kwenda kuishi Misri watakufa
kwa upanga, njaa na tauni; hakuna hata
mmoja wao atakayenusurika au kuokoka
maafa nitakayoyaleta juu yao.' 18 [f]Hili ndilo
BWANA Mwenye Nguvu Zote, Mungu wa
Israeli, asemalo: 'Kama vile hasira yangu
na ghadhabu yangu ilivyomwagwa juu
ya wale walioishi Yerusalemu, ndivyo
ghadhabu yangu itakavyomwagwa juu yenu
mtakapokwenda Misri. Mtakuwa kitu cha
kulaania na cha kutisha, cha kulaumia na
cha kushutumia, nanyi kamwe hamtaona
mahali hapa tena.'

19 [g]"Enyi mabaki ya Yuda, BWANA
amewaambia, 'Msiende Misri.' Hakikisheni
jambo hili: Ninawaonya leo 20 [h]kwamba
mmefanya kosa kubwa mioyoni mwenu
mliponituma kwa BWANA Mungu wenu
na kusema, 'Mwombe BWANA Mungu
wetu kwa ajili yetu, nawe utuambie
kila kitu atakachosema, nasi tutafanya.'
21 [i]Nimewaambieni leo, lakini bado ninyi
hamtaki kumtii BWANA Mungu wenu
katika yote aliyonituma niwaambie. 22 [j]Basi
sasa, hakikisheni jambo hili: Mtakufa kwa
upanga, njaa na tauni mahali ambapo
mnataka kwenda kuishi."

*Yeremia Apelekwa Misri*

43 [k]Yeremia alipomaliza kuwaambia
watu maneno yote ya BWANA Mungu
wao, yaani kila kitu BWANA alichokuwa
amemtuma kuwaambia, 2 [l]Azaria mwana
wa Hoshaya, na Yohanani mwana wa Karea,
na watu wote wenye kiburi wakamwambia
Yeremia, "Wewe unasema uongo! BWANA
Mungu wetu hajakutuma kusema, 'Kamwe
msiende Misri kukaa huko.' 3 [m]Lakini Baruku
mwana wa Neria anakuchochea dhidi yetu
ili ututie mikononi mwa Wakaldayo, ili
watuue au watuchukue uhamishoni Babeli."

4 [n]Basi Yohanani mwana wa Karea,
na maafisa wote wa jeshi, na watu wote
wakakataa kutii amri ya BWANA ya kukaa
katika nchi ya Yuda. 5 [o]Badala yake,
Yohanani mwana wa Karea na maafisa
wote wa jeshi wakawaongoza mabaki
yote ya Yuda waliokuwa wamerudi kuishi
katika nchi ya Yuda kutoka mataifa yote
ambayo walikuwa wametawanywa. 6 [p]Pia
wakawaongoza wanaume wote, wanawake
na watoto, na binti za mfalme ambao
Nebuzaradani kiongozi wa walinzi wa
mfalme alikuwa amewaacha na Gedalia
mwana wa Ahikamu mwana wa Shafani,
na nabii Yeremia, na Baruku mwana wa
Neria. 7 [q]Kwa hiyo wakaingia Misri kwa

[a]**42:12** Mwa 31:3; Neh 1:9; Za 106:45-46; Kut 3:21; 2Sam 24:14; 2Kor 1:3
[b]**42:13** Kum 11:28; Yer 44:16
[c]**42:14** Kum 17:16; Isa 30:2; 65:13; Hes 11:4-5; Ay 6:20; Mt 24:31; 4:2-4; Mit 10:3
[d]**42:16** Law 26:33; Eze 14:17; 11:8; Yer 41:18; Mwa 41:55; 2:17; Ay 21:20; Eze 3:16; 18:4
[e]**42:17** Yer 21:7; 44:13; 24:10
[f]**42:18** Kum 29:18-20; 2Nya 12:7; 36:19; Yer 29:18; 39:1-9; 25:18; Hes 5:27; Za 44:13
[g]**42:19** Kum 17:16; Isa 30:7; Yer 40:15; 43:2
[h]**42:20** Eze 14:7-8
[i]**42:21** Zek 7:11-12; Yer 40:3; Eze 2:7; 12:2; Kut 24:7
[j]**42:22** Yer 24:10; Eze 6:11; Isa 1:28; Yer 15:2; Hos 6:9
[k]**43:1** Yer 26:8; 42:9-22
[l]**43:2** Yer 40:16; 42:1-2; 41:16; Za 12:4; 2The 2:10-12; Neh 9:29; 1Kor 4:18-21; Mwa 19:14; 2Kor 11:31; Kum 13:3; Kut 24:7; Eze 37:18
[m]**43:3** Yer 38:4; 52:30; 32:12; 41:18
[n]**43:4** 2Nya 25:16; Yer 42:5-6, 10; 41:16
[o]**43:5** Yer 40:12
[p]**43:6** Yer 6:12; 32:12
[q]**43:7** 2Fal 25:26; Yer 2:16; 46:14; Eze 30:18

kutokumtii BWANA, wakaenda mpaka
Tahpanhesi.
8 [a]Huko Tahpanhesi neno la BWANA
likamjia Yeremia kusema: 9 [b]“Wayahudi
wakiwa wanaona, chukua baadhi ya mawe
makubwa na kuyazika katika udongo wa
mfinyanzi katika njia iliyojengwa kwa
matofali katika ingilio la jumba la kifalme la
Farao huko Tahpanhesi. 10 [c]Kisha uwaambie,
‘Hili ndilo BWANA Mwenye Nguvu Zote,
Mungu wa Israeli, asemalo: Nitamtumania
mtumishi wangu Nebukadneza mfalme wa
Babeli, nami nitakiweka kiti chake cha enzi
juu ya haya mawe niliyoyazika hapa, naye
atatandaza hema yake ya ufalme juu yake.
11 [d]Atakuja na kuishambulia Misri, akiwaua
wale waliokusudiwa kuuawa, awateke
mateka wale waliokusudiwa kutekwa,
na upanga kwa wale waliokusudiwa
upanga. 12 [e]Atachoma moto mahekalu yao
ya miungu ya Misri, atachoma mahekalu
yao na kuteka miungu yao. Kama vile
mchungaji ajizungushiavyo vazi lake ndivyo
atakavyojizungushia Misri na kuondoka
mahali hapo bila kudhurika. 13 Humo ndani
ya hekalu la jua[f] nchini ya Misri atabomoa
nguzo za ibada, na kuteketeza kwa moto
mahekalu ya miungu wa Misri.’ ”

*Maafa Kwa Sababu Ya Ibada Za Sanamu*

44 [g]Neno hili lilimjia Yeremia kuhusu
Wayahudi wote waishio Misri, huko
Migdoli, Tahpanhesi na Memfisi,[h] katika
nchi ya Pathrosi[i] kusema: 2 [j]“Hili ndilo
asemalo BWANA Mwenye Nguvu Zote,
Mungu wa Israeli: Mliona maangamizi
makubwa niliyoyaleta juu ya Yerusalemu
na juu ya miji yote ya Yuda. Leo imeachwa
ukiwa na magofu 3 [k]kwa sababu ya uovu
waliokuwa wameufanya. Walinikasirisha
kwa kufukiza uvumba na kwa kuabudu
miungu mingine ambayo kamwe wao, wala
ninyi, wala baba zenu hawakuifahamu.
4 [l]Tena na tena, niliwatuma watumishi
wangu manabii ambao walisema, ‘Msifanye
jambo hili la kuchukiza ambalo nalichukia!’
5 [m]Lakini hawakusikiliza wala hawakujali,
hawakugeuka ili kuuacha uovu wao, wala
hawakuacha kufukiza uvumba kwa miungu
mingine. 6 [n]Kwa hiyo hasira yangu kali
ilimwagika, ikawaka dhidi ya miji ya Yuda
na barabara za Yerusalemu, na kuifanya
ukiwa na magofu kama ilivyo leo.
7 [o]“Basi hili ndilo BWANA Mungu Mwenye
Nguvu Zote, Mungu wa Israeli, asemalo:
Kwa nini kujiletea maafa makubwa kama
haya juu yenu kwa kujikatilia mbali kutoka
Yuda wanaume na wanawake, watoto na
wanyonyao, hata kujiacha bila mabaki?
8 [p]Kwa nini kuichochea hasira yangu kwa
kile ambacho mikono yenu imekitengeneza,
mkaifukizia uvumba miungu mingine
huko Misri, mahali mlipokuja kuishi?
Mtajiangamiza wenyewe na kujifanya kitu
cha kulaania na shutumu miongoni mwa
mataifa yote duniani. 9 [q]Je, mmesahau uovu
uliotendwa na baba zenu, na wafalme na

[a]**43:8** Za 139:7; Yer 2:16
[b]**43:9** Mwa 31:45-53; Yos 4:1-7; 1Fal 18:31-32; Mwa 47:14
[c]**43:10** Dan 2:21; Isa 44:22; Eze 29:18-20; Yer 25:9; 27:6; 46:13; 49:38; Za 18; 11
[d]**43:11** Yer 46:13-26; Zek 11:9; Eze 32:11; 2Tim 1:7; Eze 29:19-20; Mit 11:19; Rum 6:23; Za 49:14
[e]**43:12** Kut 12:12; Zek 13:2; Za 109:18-19; 104:2; Yos 7:15; 1Fal 16:32; Isa 2:18; Yer 46:25; Eze 30:13; Dan 11:8
[f]13 Yaani Heliopoli (Mji wa Jua).
[g]**44:1** Kut 14:2; Yer 43:7-8; Isa 19:13; 11:11; Yer 46:14; Kum 32:42; Yer 24:8
[h]1 Memfisi kwa Kiebrania ni Nofu.
[i]1 Pathrosi ina maana Misri ya Juu.
[j]**44:2** Law 26:31; Kum 29:23; Mik 3:12; Yer 6:11; 40:5; 2Nya 34:24
[k]**44:3** Hes 25:3; Isa 19:1; Kum 32:17; Yer 19:4; Amu 2:19; Kut 32:22; Hes 11:33; 16:40
[l]**44:4** Yer 7:13, 25; Hes 11:29; Kum 18; 9; 1Fal 14:24; 1Pet 4:3
[m]**44:5** Yer 11:8-10; 25:4; Dan 9; 6; Mwa 6:5; 2Tim 2:19; Eze 8:18; 16:18; 23:41
[n]**44:6** Eze 8:18; 20:34; Law 26:31-34; Zek 7:14
[o]**44:7** Yer 26:19; 51:22; Hes 16:36; Rum 1:23; 2Fal 21:14
[p]**44:8** Isa 40:18-20; Rum 1:23; Yer 44:18; 1Kor 10:22; Za 44:13; Yer 41:5; Kut 12:12
[q]**44:9** Yer 11:12; 32:32; Amu 2:19; 2Fal 23:11; Mit 31:10; Yer 6:12; 1Fal 21:25

malkia wa Yuda, na uovu uliofanywa na
ninyi na wake zenu katika nchi ya Yuda
na barabara za Yerusalemu? 10 [a]Mpaka
leo hawajajinyenyekeza au kuonyesha
heshima, wala hawajafuata sheria yangu na
amri nilizoweka mbele yenu na baba zenu.
11 [b]"Kwa hiyo, hili ndilo BWANA Mwenye
Nguvu Zote, Mungu wa Israeli, asemalo:
Mimi nimekusudia kuleta maafa juu yenu,
na kuiangamiza Yuda yote. 12 [c]Nitawaondoa
mabaki ya Yuda waliokusudia kwenda Misri
kukaa humo. Wote wataangamia huko
Misri, wataanguka kwa upanga au kufa kwa
njaa. Kuanzia aliye mdogo kabisa hadi aliye
mkuu sana, watakufa kwa upanga au njaa.
Watakuwa kitu cha kulaania na cha kutisha,
cha laumu na shutumu. 13 [d]Nitawaadhibu
wale waishio Misri kwa upanga, njaa na
tauni kama nilivyoiadhibu Yerusalemu.
14 [e]Hakuna hata mmoja wa mabaki ya
Yuda ambaye amekwenda kuishi Misri
atakayeepuka au kunusurika ili kurudi
katika nchi ya Yuda, ambayo wanaitamani
sana kurudi na kuishi ndani yake, hakuna
hata mmoja atakayerudi isipokuwa
wakimbizi wachache."
15 [f]Kisha wanaume wote ambao walijua
kwamba wake zao walikuwa wakifukiza
uvumba kwa miungu mingine, pamoja
na wanawake wote waliokuwako, yaani,
kusanyiko kubwa na watu wote walioishi
nchi ya Misri na Pathrosi, wakamwambia
Yeremia, 16 [g]"Hatutausikiliza ujumbe
uliotuambia katika jina la BWANA!
17 [h]Hakika tutafanya kila kitu tulichosema
tutakifanya: Tutafukiza uvumba kwa Malkia
wa Mbinguni na tutammiminia sadaka zetu
za kinywaji kama vile sisi na baba zetu,
wafalme wetu na maafisa wetu tulivyofanya
katika miji ya Yuda na katika barabara
za Yerusalemu. Wakati ule tulikuwa na
chakula tele, tulikuwa matajiri wala
hatukupata dhara lolote. 18 [i]Lakini tangu
tulipoacha kumfukizia uvumba Malkia
wa Mbinguni na kummiminia sadaka za
kinywaji, hatupati chochote, na tumekuwa
tukiangamizwa kwa upanga na njaa."
19 [j]Wanawake wakaongeza kusema,
"Wakati tulipomfukizia uvumba Malkia
wa Mbinguni na kummiminia sadaka zetu
za kinywaji, je, waume zetu hawakujua
kwamba tulikuwa tukitengeneza maandazi
kwa mfano wake, na kummiminia yeye
sadaka za kinywaji?"
20 Ndipo Yeremia akawaambia watu
wote, wanaume na wanawake waliokuwa
wakimjibu, 21 [k]"Je, BWANA hakukumbuka
na kufikiri juu ya uvumba uliofukizwa
katika miji ya Yuda na barabara za
Yerusalemu na ninyi pamoja na baba zenu,
wafalme wenu, maafisa wenu na watu
wa nchi? 22 [l]BWANA alipokuwa hawezi
kuendelea kuvumilia matendo yenu maovu
na mambo ya machukizo mliyoyafanya,
nchi yenu ilikuwa kitu cha kulaania na
kuachwa ukiwa pasipo wakazi, kama ilivyo
leo. 23 [m]Kwa sababu mmefukiza uvumba na
kufanya dhambi dhidi ya BWANA, nanyi
hamkumtii wala kufuata sheria yake au
amri zake au maagizo yake, maafa haya
yamekuja juu yenu, kama mnavyoona
sasa."

---

[a]**44:10** Mit 28:14; Gal 3:19; 2Fal 17:17; 1Fal 9:6-9; Mt 23:12; Flp 2:9; Kum 6:13; Mt 5:17-20
[b]**44:11** 2Nya 34:24; Amo 9:4; Yer 21:10; Ufu 4:8
[c]**44:12** Yer 40:15; Isa 1:28; Zek 8:13; Yer 42:15-18; Kum 28:25; Yer 29:18
[d]**44:13** Yer 42:17; Kut 32:34; Law 26:14-17; Yer 15:2
[e]**44:14** Mao 4:15; Rum 9:27; Yer 22:24-27; 49:5; Eze 6:8
[f]**44:15** Mit 31:10; Yer 6:12; 18:15
[g]**44:16** 1Sam 8; 19; Ay 15:25-26; Mit 1:24-27; Lk 19; 14; Yer 11:8-11; 42:19
[h]**44:17** Kum 23:23; Yer 7:18; Hes 30:12; Ay 21:15; Isa 3:9; 65:3; Neh 9:34; Yer 2:26; Hes 11:4-6; Kut 16:3; Hos 2:5-13
[i]**44:18** Mal 3:13-15; Law 23:18; Yer 42:16
[j]**44:19** Yer 7:18; 18:15; Efe 5:22; Mwa 3:6; Law 7:12; Mdo 17:29
[k]**44:21** Isa 64:5; Hos 8:13; Yer 11:13; Za 79:8; Yer 14:10; 2:26
[l]**44:22** Mwa 19:13; Yer 25:18; Eze 33:28-29; Amo 2:13; Isa 1:14; Za 107:33-34
[m]**44:23** Yer 40:2; Law 26:33; Dan 9:11-12; 1Fal 9:6; Law 18:4; Yer 7:13-15; Eze 39:23

24 [a]Kisha Yeremia akawaambia watu
wote, pamoja na wanawake, “Sikieni
neno la BWANA, enyi watu wote wa Yuda
mlioko Misri. 25 [b]Hili ndilo asemalo BWANA
Mwenye Nguvu Zote, Mungu wa Israeli:
Ninyi na wake zenu mmeonyesha kwa
matendo yenu kile mlichoahidi mliposema,
‘Hakika tutatimiza nadhiri tulizoziweka za
kumfukizia uvumba na kummiminia sadaka
za kinywaji Malkia wa Mbinguni.’

“Endeleeni basi, fanyeni yale mliyoahidi!
Timizeni nadhiri zenu! 26 [c]Lakini sikieni
neno la BWANA, enyi Wayahudi wote
mnaoishi Misri: ‘Ninaapa kwa Jina langu
lililo kuu,’ asema BWANA, ‘kwamba hakuna
hata mmoja atokaye Yuda anayeishi popote
Misri ambaye kamwe ataomba tena kwa
Jina langu au kuapa, akisema, “Hakika
kama BWANA Mwenyezi aishivyo.” 27 [d]Kwa
maana ninawaangalia kwa ajili ya madhara,
wala sio kwa mema. Wayahudi walioko
Misri wataangamia kwa upanga na njaa,
hadi wote watakapoangamizwa. 28 [e]Wale
watakaonusurika upanga na kurudi katika
nchi ya Yuda kutoka Misri watakuwa
wachache sana. Ndipo mabaki wote wa
Yuda waliokuja kuishi Misri watakapojua
ni neno la nani litakalosimama, kwamba
ni langu au lao.

29 [f]“ ‘Hii itakuwa ndiyo ishara kwenu
kwamba nitawaadhibu mahali hapa, asema
BWANA, ili mpate kujua kuwa onyo langu
la madhara dhidi yenu hakika litatimizwa.’
30 [g]Hili ndilo asemalo BWANA: ‘Nitamtia
Farao Hofra mfalme wa Misri mikononi
mwa adui zake wanaoutafuta uhai wake,
kama vile nilivyomtia Sedekia mfalme wa
Yuda mikononi mwa Nebukadneza mfalme
wa Babeli, adui aliyekuwa akiutafuta uhai
wake.’ ”

*Ujumbe Kwa Baruku*

45 [h]Hili ndilo nabii Yeremia alilomwambia
Baruku mwana wa Neria katika mwaka
wa nne wa utawala wa Yehoyakimu mwana
wa Yosia mfalme wa Yuda, baada ya Baruku
kuandika katika kitabu maneno ambayo
yalitoka kinywani mwa Yeremia wakati
ule: 2 “Hili ndilo BWANA, Mungu wa Israeli,
akuambialo wewe Baruku: 3 [i]Ulisema, ‘Ole
wangu! BWANA ameongeza huzuni juu ya
maumivu yangu, nimechoka kwa kulia kwa
uchungu wala sipati pumziko.’ ”

4 [j]BWANA akasema, “Mwambie hivi:
‘Hili ndilo asemalo BWANA: Nitakibomoa
kile nilichokijenga, na kung’oa kile
nilichokipanda katika nchi yote. 5 [k]Je,
utajitafutia mambo makubwa kwa ajili
yako mwenyewe? Usiyatafute hayo.
Kwa kuwa nitaleta maangamizi juu ya
watu wote, asema BWANA, lakini popote
utakapokwenda, nitayaokoa maisha yako.’ ”

*Ujumbe Kuhusu Misri*

46 [l]Hili ni neno la BWANA lililomjia nabii
Yeremia kuhusu mataifa:

2 [m]Kuhusu Misri:

Huu ni ujumbe dhidi ya jeshi la Farao
Neko mfalme wa Misri, lililoshindwa
huko Karkemishi kwenye Mto Frati na
Nebukadneza mfalme wa Babeli, katika
mwaka wa nne wa utawala wa Yehoyakimu
mwana wa Yosia mfalme wa Yuda:

[a]**44:24** Mwa 3:6; Yer 43:7
[b]**44:25** Kum 32:28; Mit 20:25; Yak 1:13-15; Mit 31:10; Eze 20:29
[c]**44:26** Mwa 22:16; Mdo 19:13; Za 50:16; Kum 32:40; Yer 24:8; Ebr 6:13-17; Mwa 15:2
[d]**44:27** Yer 21:10; 31:28; Eze 7:6; Yer 1:12; Ay 15:22; 2Pet 3:8-9; Dan 9:14; Amo 9:8
[e]**44:28** Isa 27:13; 10:19; Hab 3:2; Yer 45:5; Eze 6:8; Yer 39:16; 42:15-18
[f]**44:29** Mwa 24:14; Kut 3:12; Hes 16:38; Mt 12:38; Mit 19:21
[g]**44:30** Eze 29:3; Yer 25:19; Eze 32:32; Yer 24:8; 43:9-13; 2Fal 25:1-7
[h]**45:1** Yer 32:12; 36:18, 32; Isa 50:4; Yer 51:59; Kut 17:14; Za 40:7; 2Nya 36:5
[i]**45:3** Ay 23:2; Za 69:3; Isa 24:16; 1Kor 9:16; Mk 14:34; Rum 9:2; Ay 6:10; Ebr 4:3; Mt 11:24
[j]**45:4** Isa 5:5; Yer 11:17; Kum 30:9; Yer 42:10; 18:7-10; Kum 28:63
[k]**45:5** Mt 6:25-27, 33; Yer 21:9; 32:8; 11:11; 40:2; 2:35; Za 68:20
[l]**46:1** Yer 25:15-38; 1:10
[m]**46:2** 2Fal 23:29; 2Nya 35:20; Mwa 2:14

3 [a]"Wekeni tayari ngao zenu, kubwa
na ndogo,
mtoke kwa ajili ya vita!
4 [b]Fungieni farasi lijamu,
pandeni farasi!
Shikeni nafasi zenu
mkiwa mmevaa chapeo!
Isugueni mikuki yenu,
vaeni dirii vifuani!
5 [c]Je, ninaona nini?
Wametiwa hofu,
wanarudi nyuma,
askari wao wameshindwa.
Wanakimbia kwa haraka
pasipo kutazama nyuma,
tena kuna hofu kuu kila upande,"
asema BWANA.
6 [d]Walio wepesi na wenye mbio
hawawezi kukimbia,
wala wenye nguvu hawawezi
kutoroka.
Kaskazini, kando ya Mto Frati,
wanajikwaa na kuanguka.

7 [e]"Ni nani huyu ajiinuaye kama Mto
Naili,
kama mito yenye maji
yanayofanya mawimbi?
8 [f]Misri hujiinua kama Mto Naili,
kama mito yenye maji
yanayofanya mawimbi.
Husema, 'Nitainuka na kufunika
dunia,
nitaiangamiza miji na watu wake.'
9 [g]Songeni mbele, enyi farasi!
Endesheni kwa ukali, enyi magari
ya farasi,
Endeleeni mbele, enyi mashujaa:
watu wa Kushi[h] na Putu[i]
wachukuao ngao,
watu wa Ludi[j] wavutao upinde.
10 [k]Lakini ile siku ni ya Bwana, BWANA
Mwenye Nguvu Zote,
siku ya kulipiza kisasi,
kisasi juu ya adui zake.
Upanga utakula hata
utakapotosheka,
hadi utakapozima kiu yake kwa
damu.
Kwa maana Bwana, BWANA Mwenye
Nguvu Zote, atatoa dhabihu
kwenye nchi ya kaskazini, kando
ya Mto Frati.

11 [l]"Panda hadi Gileadi ukapate zeri,
ee Bikira Binti wa Misri.
Lakini umetumia dawa nyingi bila
mafanikio;
huwezi kupona.
12 [m]Mataifa yatasikia juu ya aibu yako,
kilio chako kitaijaza dunia.
Shujaa mmoja atajikwaa juu ya
mwingine,
nao wataanguka chini pamoja."

13 [n]Huu ndio ujumbe BWANA aliomwambia nabii Yeremia kuhusu kuja kwa Nebukadneza mfalme wa Babeli ili kuishambulia Misri:

14 [o]"Tangaza hili katika Misri, nawe
ulihubiri katika Migdoli,
hubiri pia katika Memfisi[p] na
Tahpanhesi:[q]

---

[a]**46:3** Isa 21:5; Yer 51:11-12; Isa 8:9-10; Yoe 3:9-10
[b]**46:4** Eze 21:9-11; 2Nya 26:14; Neh 4:16; 1Sam 17:5, 38
[c]**46:5** Yer 48:44; Za 31:13; Yer 49:29; Ufu 6:15-17
[d]**46:6** Isa 30:16; Za 20:8; Dan 11:19; Mwa 2:14; 15:18
[e]**46:7** Dan 11:22; Yer 47:2
[f]**46:8** Dan 11:10; Eze 29:3, 9; 30:12; Amo 8:8
[g]**46:9** Mwa 10:6; Yer 47:3; Isa 66:19; Eze 26:10

[h]9 Kushi ni Naili ya Juu; sasa ni Sudan.
[i]9 Putu sasa ni Libya.
[j]9 Nchi iliyo Afrika ya Kaskazini, magharibi ya Mto Naili; sasa ni Libya.
[k]**46:10** Eze 32:10; Mao 1:15; Hes 31:3; 2Fal 23:29-30; Law 3:9; Isa 34:6
[l]**46:11** Yer 8:22; Mwa 37:35; 2Fal 19:21; Isa 47:1; Yer 30:13
[m]**46:12** Isa 19:4; Nah 3:8-10
[n]**46:13** Yer 43:10; Isa 19:1; Yer 27:7; Eze 32:11
[o]**46:14** Yer 43:8; Isa 19:13; 2Sam 2:26; Kum 32:42; Yer 24:8
[p]14 Memfisi kwa Kiebrania ni Nofu.
[q]14 Ni mji katika Misri.

'Shikeni nafasi zenu na mwe tayari,
kwa kuwa upanga unawala wale
wanaokuzunguka.'
15 [a]Kwa nini mashujaa wako
wamesombwa
na kupelekwa mbali?
Hawawezi kusimama, kwa maana
Bwana
atawasukuma awaangushe chini.
16 [b]Watajikwaa mara kwa mara,
wataangukiana wao kwa wao.
Watasema, 'Amka, turudi
kwa watu wetu na nchi yetu,
mbali na upanga wa mtesi.'
17 [c]Huko watatangaza,
'Farao mfalme wa Misri ni
makelele tu,
amekosa wasaa wake.'

18 [d]"Kwa hakika kama niishivyo,"
asema Mfalme,
ambaye jina lake ni Bwana
Mwenye Nguvu Zote,
"mmoja atakuja ambaye ni kama
Tabori miongoni mwa milima,
kama Karmeli kando ya bahari.
19 [e]Funga mizigo yako kwenda
uhamishoni,
wewe ukaaye Misri,
kwa kuwa Memfisi utaangamizwa
na kuwa magofu pasipo mkazi.

20 [f]"Misri ni mtamba mzuri,
lakini kipanga anakuja dhidi yake
kutoka kaskazini.
21 [g]Askari wake waliokodiwa katika
safu zake
wako kama ndama
walionenepeshwa.
Wao pia watageuka na kukimbia
pamoja,
hawataweza kuhimili vita,
kwa maana siku ya msiba inakuja
juu yao,
wakati wao wa kuadhibiwa.
22 [h]Misri atatoa sauti kama ya nyoka
anayekimbia
kadiri adui anavyowasogelea na
majeshi,
watakuja dhidi yake wakiwa na
mashoka,
kama watu wakatao miti.
23 [i]Wataufyeka msitu wake,"
asema Bwana,
"hata kama umesongamana kiasi
gani.
Ni wengi kuliko nzige,
hawawezi kuhesabika.
24 [j]Binti wa Misri ataaibishwa,
atatiwa mikononi mwa watu wa
kaskazini."

25 [k]Bwana Mwenye Nguvu Zote, Mungu
wa Israeli, asema: "Nakaribia kuleta adhabu
juu ya Amoni mungu wa Thebesi,[l] na juu ya
Farao, Misri na miungu yake, na wafalme
wake, pamoja na wale wanaomtegemea
Farao. 26 [m]Nitawatia mikononi mwa wale
wanaotafuta uhai wao, yaani Nebukadneza
mfalme wa Babeli na maafisa wake.
Hatimaye, hata hivyo, Misri itakaliwa kama
nyakati zilizopita," asema Bwana.

27 [n]"Usiogope, ee Yakobo mtumishi
wangu,
usifadhaike, ee Israeli.
Hakika nitakuokoa kutoka nchi za
mbali,
uzao wako kutoka nchi ya
uhamisho wao.

---

[a]**46:15** Yos 23:5; Isa 66:15-16
[b]**46:16** Law 26:37; Isa 13:14; Yer 25:38
[c]**46:17** Isa 19:11-16; 1Fal 20:10-11
[d]**46:18** Yer 48:15; Yos 19:22; 1Fal 18:42
[e]**46:19** Yer 48:18; Isa 20:4; 19:13; Eze 29:10-12; 35:7
[f]**46:20** Isa 14:31; Hos 10:11; Yer 47:2
[g]**46:21** 2Fal 7:6; Ay 20:24; Za 18:18; Yer 18:17; Lk 15:27; Ay 18:20; Za 37:13
[h]**46:22** Za 74:5
[i]**46:23** Isa 29:4; Amo 7:12; Za 74:5; Kum 28:42
[j]**46:24** 2Fal 24:7; Yer 1:15
[k]**46:25** Eze 30:14; Nah 3:4; Yer 43:12; Isa 20:6; Eze 30:22; 2Fal 24:7
[l]25 Thebesi kwa Kiebrania ni No (au No-Amoni), mji katika Misri.
[m]**46:26** Yer 44:30; Isa 19:4; Eze 32:11; 29:11-16
[n]**46:27** Yer 29:14; Isa 41:13; Yer 51:46; Isa 11:11; 43:5; 41:8; Yer 50:19

Yakobo atakuwa tena na amani na salama,
wala hakuna hata mmoja atakayewatia hofu.
28 [a]Usiogope, ee Yakobo mtumishi wangu,
kwa maana mimi niko pamoja nawe,”
asema BWANA.
“Ingawa nitayaangamiza kabisa mataifa yote
ambayo miongoni mwake nimekutawanya,
sitakuangamiza wewe kabisa.
Nitakurudi, lakini kwa haki tu,
wala sitakuacha kabisa bila kukuadhibu.”

*Ujumbe Kuhusu Wafilisti*

47 [b]Hili ndilo neno la BWANA lililomjia nabii Yeremia kuhusu Wafilisti, kabla Farao hajaishambulia Gaza:
2 [c]Hili ndilo asemalo BWANA:

“Tazama jinsi maji yanavyoinuka huko kaskazini,
yatakuwa mafuriko yenye nguvu sana.
Yataifurikia nchi na vitu vyote vilivyomo ndani yake,
miji na wale waishio ndani yake.
Watu watapiga kelele;
wote waishio katika nchi wataomboleza
3 [d]kwa sauti ya kwato za farasi waendao mbio,
kwa sauti ya magari ya adui
na mngurumo wa magurudumu yake.
Baba hawatageuka kuwasaidia watoto wao,
mikono yao italegea.
4 [e]Kwa maana siku imewadia kuwaangamiza Wafilisti wote
na kuwakatilia mbali walionusurika wote
ambao wangeweza kusaidia Tiro na Sidoni.
BWANA anakaribia kuwaangamiza Wafilisti,
mabaki toka pwani za Kaftori.[f]
5 [g]Gaza atanyoa kichwa chake katika kuomboleza,
Ashkeloni atanyamazishwa.
Enyi mabaki kwenye tambarare,
mtajikatakata wenyewe mpaka lini?

6 [h]“Mnalia, ‘Aa, upanga wa BWANA,
utaendelea mpaka lini ndipo upumzike?
Rudi ndani ya ala yako;
acha na utulie.’
7 [i]Lakini upanga utatuliaje
wakati BWANA ameuamuru,
wakati ameuagiza kuishambulia Ashkeloni
pamoja na pwani yake?”

*Ujumbe Kuhusu Moabu*

48 [j]Kuhusu Moabu:

Hili ndilo BWANA Mwenye Nguvu Zote, Mungu wa Israeli, asemalo:

“Ole wake Nebo, kwa maana utaharibiwa.
Kiriathaimu utaaibishwa na kutekwa;
Misgabu itaaibishwa na kuvunjavunjwa.

---

[a]**46:28** Kut 14:22; Hes 14:9; Yer 4:27; Isa 8:9-10
[b]**47:1** Zek 9:5-7; Sef 2:4-5; Amo 1:6; Mwa 10:14-19
[c]**47:2** Isa 8:7; 14:31; 15:3
[d]**47:3** Yer 46:9; Eze 23:24; Yer 50:43; Eze 7:17; 21:7
[e]**47:4** Isa 23:1; Amo 1:9-10; Mwa 10:14-15; Yer 25:22; Yoe 3:4; Kum 2:23; Za 9:2-4
[f]4 Kaftori ndio Krete.
[g]**47:5** Yer 41:5; Mik 1:16; Yer 25:20; Law 19:28
[h]**47:6** Isa 34:5; Yer 12:12; Eze 21:3; Yer 48:10; 50:35
[i]**47:7** Eze 25:15-17
[j]**48:1** Hes 32:37; Yos 13:19; Mwa 19:37; Kum 23:6

2 [a]Moabu haitasifiwa tena;
huko Heshboni watu watafanya shauri baya la anguko lake:
'Njooni na tuangamize taifa lile.'
Wewe nawe, ee Madmena, utanyamazishwa;
upanga utakufuatia.
3 Sikiliza kilio kutoka Horonaimu,
kilio cha maangamizi makuu na uharibifu.
4 Moabu utavunjwa,
wadogo wake watapiga kelele.
5 [b]Wanapanda kwenda njia ya kuelekea Luhithi,
wakilia kwa uchungu wanapotembea,
kwenye njia inayoshuka kwenda Horonaimu,
kilio cha uchungu kwa ajili ya uharibifu kinasikika.
6 [c]Kimbieni! Okoeni maisha yenu,
kuweni kama kichaka jangwani.
7 [d]Kwa kuwa mmetumainia matendo yenu na mali zenu,
ninyi pia mtachukuliwa mateka,
naye Kemoshi[e] atakwenda uhamishoni,
pamoja na makuhani wake na maafisa wake.
8 [f]Mharabu atakuja dhidi ya kila mji,
wala hakuna mji utakaookoka.
Bonde litaangamizwa na uwanda utaharibiwa,
kwa sababu BWANA amesema.
9 [g]Wekeni chumvi kwa ajili ya Moabu,
kwa kuwa ataangamizwa;
miji yake itakuwa ukiwa,
pasipo kuwa na mtu atakayeishi ndani yake.

10 [h]"Alaaniwe yeye afanyaye kazi ya BWANA kwa hila!
Alaaniwe yeye auzuiaye upanga wake usimwage damu!

11 [i]"Moabu amestarehe tangu ujana wake,
kama divai iliyoachwa kwenye machujo yake,
haikumiminwa kutoka chombo kimoja hadi kingine,
hajaenda uhamishoni.
Kwa hiyo ana ladha ile ile kama aliyokuwa nayo,
nayo harufu yake haijabadilika.
12 Lakini siku zinakuja,"
asema BWANA,
"nitakapotuma watu wamiminao kutoka kwenye magudulia,
nao watamimina;
wataacha magudulia yake yakiwa matupu
na kuvunja mitungi yake.
13 [j]Kisha Moabu atamwonea aibu mungu wao Kemoshi,
kama vile nyumba ya Israeli walivyoona aibu
walipotegemea mungu wa Betheli.[k]

14 [l]"Mwawezaje kusema, 'Sisi ni mashujaa,
watu jasiri katika vita'?
15 [m]Moabu ataangamizwa na miji yake itavamiwa,
vijana wake waume walio bora sana watachinjwa,"
asema Mfalme, ambaye jina lake
ni BWANA Mungu Mwenye Nguvu Zote.

---

[a]**48:2** Hes 21:25; Isa 16:14; Yos 23:16
[b]**48:5** Isa 15:5
[c]**48:6** Yer 17:6; Mwa 19:17
[d]**48:7** Hes 21:29; Isa 46:1-2; Yer 49:3; 9:23; Za 49:6; Mk 11:28; Amo 2:3
[e]7 Kemoshi alikuwa mungu wa Wamoabu.
[f]**48:8** Kut 12:23; Yer 4:7; Yos 13:9
[g]**48:9** Amu 9:45; Yer 51:29
[h]**48:10** Yer 47:6; 1Fal 20:42; 1Sam 15:3, 11; 2Fal 13:15-19
[i]**48:11** Zek 1:15; Sef 1:12
[j]**48:13** Hos 10:6; Amu 11:24; Yos 7:2
[k]13 Betheli ina maana ya Nyumba ya Mungu; lakini pia ni mahali ambapo Mfalme Yeroboamu alisimamisha moja ya sanamu za ndama ili kuabudiwa; nyingine aliiweka huko Dani (1Fal 12:29-33).
[l]**48:14** Mhu 9:11; Za 33:16
[m]**48:15** Yer 50:27; 51:40, 57; 46:18; Isa 9:17

16 “Kuanguka kwa Moabu kumekaribia,
janga kubwa litamjia kwa haraka.
17 [a]Ombolezeni kwa ajili yake, ninyi
nyote mnaomzunguka,
ninyi nyote mnaojua sifa zake,
semeni, ‘Tazama jinsi ilivyovunjika
fimbo ya kifalme yenye
nguvu,
tazama jinsi ilivyovunjika fimbo
iliyotukuka!’

18 [b]“Shuka kutoka fahari yako
na uketi katika ardhi iliyokauka,
enyi wenyeji wa Binti wa Diboni,
kwa maana yeye aangamizaye
Moabu atakuja dhidi yako,
na kuangamiza miji yako
iliyozungushiwa maboma.
19 [c]Simama kando ya barabara na
utazame,
wewe unayeishi Aroeri.
Muulize mwanaume anayekimbia
na mwanamke anayetoroka,
waulize, ‘Kumetokea nini?’
20 [d]Moabu amefedheheshwa, kwa kuwa
amevunjavunjwa.
Lieni kwa huzuni na kupiga kelele!
Tangazeni kando ya Arnoni
kwamba Moabu ameangamizwa.
21 [e]Hukumu imefika kwenye uwanda
wa juu:
katika Holoni, Yahasa na
Mefaathi,
22 [f]katika Diboni, Nebo
na Beth-Diblathaimu,
23 [g]katika Kiriathaimu, Beth-Gamuli
na Beth-Meoni,
24 [h]katika Keriothi na Bosra;
kwa miji yote ya Moabu,
iliyoko mbali na karibu.
25 [i]Pembe[j] ya Moabu imekatwa,
mkono wake umevunjwa,”
asema Bwana.

26 [k]“Mlevye,
kwa kuwa amemdharau Bwana.
Moabu na agaegae katika matapishi
yake,
yeye na awe kitu cha dhihaka.
27 [l]Je, Israeli hakuwa kitu chako cha
kudhihakiwa?
Je, alikamatwa miongoni mwa
wezi,
kiasi cha kutikisa kichwa chako kwa
dharau
kila mara unapozungumza juu
yake?
28 [m]Ondokeni kwenye miji yenu,
mkaishi katikati ya miamba,
enyi mnaoishi Moabu.
Kuweni kama huwa ambaye
hutengeneza kiota chake
kwenye mdomo wa pango.

29 [n]“Tumesikia juu ya kiburi cha
Moabu:
kutakabari kwake kwa kiburi na
majivuno,
kiburi chake na ufidhuli wake,
na kujivuna kwa moyo wake.
30 Ninaujua ujeuri wake, lakini ni
bure,”
asema Bwana,
“nako kujisifu kwake hakumsaidii
chochote.
31 [o]Kwa hiyo namlilia Moabu,
kwa ajili ya Moabu yote ninalia,
ninaomboleza kwa ajili
ya watu wa Kir-Haresethi.

[a]**48:17** Za 110:2; 2Fal 3:4-5
[b]**48:18** Isa 47:1; Hes 21:30; Yos 13:9
[c]**48:19** Hes 32:34; Kum 2:36
[d]**48:20** Isa 16:7; Hes 21:13
[e]**48:21** Hes 21:23; Isa 15:4; Yos 13:18; 15:51; 13:9, 21
[f]**48:22** Hes 21:30; Yos 13:9, 17; Hes 32:38
[g]**48:23** Hes 32:38; Yos 13:17-19
[h]**48:24** Amo 2:2; Yer 49:13; Isa 15:1
[i]**48:25** Za 75:10; Eze 30:21; Za 37:17
[j]25 Pembe hapa ni ishara ya nguvu.
[k]**48:26** Yer 25:16, 27; 51:39; Isa 28:8; 1Sam 17:26
[l]**48:27** Mit 24:17; Yer 2:26; Ay 16:4; Za 44:14; Mik 7:8-10; Kum 7:8-10; Sef 2:8
[m]**48:28** Za 55:6-7; Wim 1:15; Amu 6:2; Wim 2:14; Mwa 8; 8
[n]**48:29** Law 26:19; Isa 16:6; Ay 40:12; Mit 10:5; 16:18
[o]**48:31** Isa 15:5-6; 2Fal 3:25

32 [a]Ninalia machozi kwa ajili yenu,
kama Yazeri aliavyo,
enyi mizabibu ya Sibma.
Matawi yako yameenea hadi
baharini;
yamefika hadi bahari ya Yazeri.
Mharabu ameyaangukia matunda
yako yaliyoiva
na mizabibu yako iliyoiva.
33 [b]Shangwe na furaha vimetoweka
kutoka bustani na mashamba ya
Moabu.
Nimekomesha kutiririka kwa divai
kutoka mashinikizo;
hakuna hata mmoja ayakanyagaye
kwa kelele za shangwe.
Ingawa kuna kelele,
sio kelele za shangwe.

34 [c]"Sauti ya kilio chao inapanda
kutoka Heshboni hadi Eleale na
Yahazi,
kutoka Soari hadi Horonaimu na
Eglath-Shelishiya,
kwa kuwa hata maji ya Nimrimu
yamekauka.
35 [d]Nitakomesha wale wote katika
Moabu
watoao sadaka mahali pa juu,
na kufukiza uvumba kwa miungu
yao,"
asema Bwana.
36 [e]"Kwa hiyo moyo wangu
unaomboleza kwa ajili ya
Moabu kama filimbi;
unaomboleza kama filimbi kwa
ajili ya watu wa Kir-Haresethi.
Utajiri waliojipatia umetoweka.
37 [f]Kila kichwa kimenyolewa
na kila mwenye ndevu zimekatwa;
kila mkono umekatwa
na kila kiuno kimefunikwa kwa
nguo ya gunia.
38 [g]Juu ya mapaa yote katika Moabu
na katika viwanja
hakuna kitu chochote isipokuwa
maombolezo,
kwa kuwa nimemvunja Moabu
kama gudulia ambalo hakuna mtu
yeyote anayelitaka,"
asema Bwana.
39 "Tazama jinsi alivyovunjikavunjika!
Jinsi wanavyolia kwa huzuni!
Tazama jinsi Moabu anavyogeuka
kwa aibu!
Moabu amekuwa kitu cha
kudhihakiwa,
kitu cha kutisha kwa wale wote
wanaomzunguka."

40 [h]Hili ndilo asemalo Bwana:

"Tazama! Tai anashuka chini,
akitanda mabawa yake juu ya
Moabu.
41 [i]Miji itatekwa na ngome zake
zitatwaliwa.
Katika siku hiyo, mioyo ya mashujaa
wa Moabu
itakuwa kama moyo wa
mwanamke katika utungu wa
kuzaa.
42 [j]Moabu ataangamizwa kama taifa
kwa sababu amemdharau Bwana.
43 [k]Hofu kuu, shimo na mtego
vinawangojea,
enyi watu wa Moabu,"
asema Bwana.
44 [l]"Yeyote atakayeikimbia hiyo hofu
kuu
ataanguka ndani ya shimo,
yeyote atakayepanda kutoka
shimoni,
atanaswa katika mtego,
kwa sababu nitaletea Moabu
mwaka wa adhabu yake,"

---

[a]**48:32** Hes 32:3; 21:13; Isa 16:8-9; Yos 13:25
[b]**48:33** Isa 16:10; 24:7; Amo 5:17; Yoe 1:12
[c]**48:34** Isa 15:4-6; Hes 32:3; 21:23; Mwa 13:10; Yos 13:26; Hes 21:25
[d]**48:35** Isa 15:2; 16:12; Yer 11:13
[e]**48:36** Isa 16:11; 15:7; Mit 11:4; 2Fal 3:25
[f]**48:37** Isa 15:2; Eze 29:18; Isa 3:24; Amo 8:10; Eze 27:31; 2Sam 10:4
[g]**48:38** Yer 22:28; Isa 15:3
[h]**48:40** Kum 28:29; Hab 1:8; Isa 8:8; Yer 49:22
[i]**48:41** Isa 21:3; Mik 4:9; Amo 2:16; Isa 15:1
[j]**48:42** Za 83:4; Isa 16:14; Mit 16:18
[k]**48:43** Isa 24:17, 18; Yer 49:5
[l]**48:44** 1Fal 19:17; Ay 20:24; Yer 11:23; 23:12; Isa 24:18

asema BWANA.

45 [a]"Katika kivuli cha Heshboni,
wakimbizi wamesimama pasipo msaada,
kwa kuwa moto umezimika huko Heshboni,
mwali wa moto kutoka katikati ya Sihoni;
unaunguza vipaji vya nyuso za Moabu,
mafuvu yao wenye kujivuna kwa kelele.
46 [b]Ole wako, ee Moabu!
Watu wa Kemoshi wameangamizwa;
wana wako wamepelekwa uhamishoni
na binti zako wamechukuliwa mateka.

47 [c]"Lakini nitarudisha mateka wa Moabu,
katika siku zijazo,"
asema BWANA.

Huu ndio mwisho wa hukumu juu ya Moabu.

*Ujumbe Kuhusu Amoni*

49 [d]Kuhusu Waamoni:

Hili ndilo asemalo BWANA:

"Je, Israeli hana wana?
Je, hana warithi?
Kwa nini basi Moleki amechukua milki ya Gadi?
Kwa nini watu wake wanaishi katika miji yake?
2 [e]Lakini siku zinakuja,"
asema BWANA,
"nitakapopiga kelele ya vita
dhidi ya Raba mji wa Waamoni;
utakuwa kilima cha magofu,
navyo vijiji vinavyouzunguka
vitateketezwa kwa moto.
Kisha Israeli atawafukuza
wale waliomfukuza,"
asema BWANA.
3 [f]"Lia kwa huzuni, ee Heshboni, kwa kuwa Ai umeangamizwa!
Pigeni kelele, enyi wakazi wa Raba!
Vaeni nguo za gunia na kuomboleza,
kimbieni hapa na pale ndani ya kuta,
kwa kuwa Moleki atakwenda uhamishoni,
yeye pamoja na makuhani na maafisa wake.
4 [g]Kwa nini unajivunia mabonde yako,
kujivunia mabonde yako yaliyozaa sana?
Ee binti usiye mwaminifu,
unayeutumainia utajiri wako na kusema,
'Ni nani atakayenishambulia?'
5 [h]Nitaleta hofu kuu juu yako
kutoka kwa wale wote wanaokuzunguka,"
asema Bwana, BWANA Mwenye Nguvu Zote.
"Kila mmoja wenu ataondolewa,
wala hakuna hata mmoja atakayekusanya wakimbizi.

6 [i]"Lakini hatimaye,
nitarudisha mateka wa Waamoni,"
asema BWANA.

*Ujumbe Kuhusu Edomu*

7 [j]Kuhusu Edomu:

Hili ndilo asemalo BWANA Mwenye Nguvu Zote:

[a]**48:45** Hes 21:21, 26-28; Yos 12:2; Hes 24:17
[b]**48:46** Hes 21:29; Amu 11:24
[c]**48:47** Za 14:7; Dan 11:41; Yer 49:6; Isa 11:1; Yer 12:15; Eze 16:53
[d]**49:1** Amo 1:13; Mwa 19:38; 1Sam 11:1-11; 2Sam 10:1-9; Law 18:21; Mwa 30:11
[e]**49:2** Yer 4:19; Kum 3:11; Isa 1:2; Eze 25:2-11; Kum 13:16; Yer 30:16; Eze 21:28-32
[f]**49:3** Mwa 12:8; Yos 8:28; 13:26; Mwa 37:34
[g]**49:4** Yer 21:13; 9:23; 1Tim 6:17; Yer 3:6
[h]**49:5** Yer 44:14
[i]**49:6** Yer 12:14-17; 48:47
[j]**49:7** Ay 5:12-14; Za 83:6; Eze 25:12; Mwa 36:11-15, 34; 25:30

“Je, hakuna tena hekima katika
Temani?
Je, shauri limewapotea wenye
busara?
Je, hekima yao imechakaa?
8 [a]Geuka na ukimbie, jifiche katika
mapango marefu kabisa,
wewe uishiye Dedani,
kwa kuwa nitaleta maafa juu ya Esau
wakati nitakapomwadhibu.
9 Je, kama wachuma zabibu
wangekuja kwako,
wasingebakiza zabibu chache?
Kama wezi wangekujia usiku,
je, si wangeiba tu kiasi ambacho
wangehitaji?
10 [b]Lakini nitamvua Esau nguo abaki
uchi,
nitayafunua maficho yake,
ili asiweze kujificha.
Watoto wake, jamaa na majirani
wataangamia,
naye hatakuwepo tena.
11 [c]Waache yatima wako; nitayalinda
maisha yao.
Wajane wako pia
wanaweza kunitumaini mimi.”

12 [d]Hili ndilo asemalo BWANA: “Kama
wale wasiostahili kukinywea kikombe
ni lazima wakinywe, kwa nini wewe
usiadhibiwe? Hutakwepa kuadhibiwa, ni
lazima ukinywe. 13 [e]Ninaapa kwa nafsi
yangu,” asema BWANA, “kwamba Bosra
utakuwa magofu na kitu cha kutisha,
cha aibu na cha kulaania; miji yake yote
itakuwa magofu milele.”

14 Nimesikia ujumbe kutoka kwa
BWANA:
Mjumbe alitumwa kwa mataifa
kusema,
“Jikusanyeni ili kuushambulia!
Inukeni kwa ajili ya vita!”

15 “Sasa nitakufanya uwe mdogo
miongoni mwa mataifa,
aliyedharauliwa miongoni mwa
watu.
16 [f]Vitisho vyako na kiburi cha moyo
wako
vimekudanganya,
wewe unayeishi katika majabali ya
miamba,
wewe unayedumu katika miinuko
ya kilima.
Ujapojenga kiota chako juu sana
kama cha tai,
nitakushusha chini kutoka huko,”
asema BWANA.
17 [g]“Edomu atakuwa kitu cha kuogofya;
wote wapitao karibu
watashangaa na kuzomea
kwa sababu ya majeraha yake
yote.
18 [h]Kama vile Sodoma na Gomora
zilivyoangamizwa,
pamoja na miji iliyokuwa jirani
nayo,”
asema BWANA,
“vivyo hivyo hakuna mtu yeyote
atakayeishi humo.
Naam, hakuna mtu yeyote
atakayekaa humo.

19 [i]“Kama simba anayepanda kutoka
vichaka vya Yordani
kuja kwenye nchi ya malisho
mengi,
ndivyo nitamfukuza Edomu kutoka
nchi yake ghafula.
Ni nani aliye mteule

[a]**49:8** Mwa 10:7; Yer 25:23; Isa 2:19; Amu 6:2; Mwa 25:3
[b]**49:10** Eze 35:4; Isa 17:14; Mao 1:18; Mwa 3:8; Isa 34:10-12; Yer 11:23
[c]**49:11** Hos 14:3; Mit 23:10-11; Kum 10:18; Yak 1:27
[d]**49:12** Isa 51:23; Mt 20:22; Mit 11:31; Yer 25:28-29; 25:15
[e]**49:13** Mwa 22:16; 36:33; Isa 34:6; Yer 42:18; Eze 35:9; Yer 42:18
[f]**49:16** Ay 39:27-28; Amo 9:2; Eze 35:13; Oba 1:12
[g]**49:17** Kum 29:22; Yer 50:13; Eze 35:7
[h]**49:18** Mwa 19:24; Kum 29:23; Amo 4:11; Isa 34:10; Yer 23:14
[i]**49:19** Yer 12:5; Ay 9:19; Yer 50:44; Za 89:6-8; 1Sam 17:34; Kut 8:10; 2Nya 20:6

nitakayemweka kwa ajili ya
jambo hili?
Ni nani aliye kama mimi,
na ni nani awezaye kunipinga?
Tena ni mchungaji yupi awezaye
kusimama kinyume nami?"
20 [a]Kwa hiyo, sikia kile BWANA
alichokipanga dhidi ya
Edomu,
kile alichokusudia dhidi ya wale
waishio Temani:
Aliye mchanga katika kundi
ataburutwa mbali;
yeye ataharibu kabisa malisho yao
kwa sababu yao.
21 [b]Kwa sauti ya anguko lao, dunia
itatetemeka.
Kilio chao kitasikika hadi Bahari
ya Shamu.[c]
22 [d]Tazama! Tai atapaa juu angani na
kuruka chini kwa ghafula,
akitandaza mabawa yake juu ya
Bosra.
Katika siku hiyo, mioyo ya mashujaa
wa Edomu
itakuwa kama moyo wa
mwanamke katika utungu wa
kuzaa.

*Ujumbe Kuhusu Dameski*

23 [e]Kuhusu Dameski:

"Hamathi na Arpadi imetahayarika,
kwa kuwa wamesikia habari
mbaya.
Wamevunjika moyo na wametaabika
kama bahari iliyochafuka.
24 [f]Dameski amedhoofika,
amegeuka na kukimbia,
hofu ya ghafula imemkamata sana;
amepatwa na uchungu na maumivu,
maumivu kama ya mwanamke
katika utungu wa kuzaa.
25 Kwa nini mji ambao unajulikana
haujaachwa,
mji ambao ninaupenda?
26 [g]Hakika, vijana wake wanaume
wataanguka barabarani;
askari wake wote
watanyamazishwa siku hiyo,"
asema BWANA Mwenye Nguvu Zote.
27 [h]"Nitatia moto kuta za Dameski;
utaangamiza ngome za
Ben-Hadadi."

*Ujumbe Kuhusu Kedari Na Hazori*

28 [i]Kuhusu Kedari na falme za Hazori, ambazo Nebukadneza mfalme wa Babeli alizishambulia:

Hili ndilo asemalo BWANA:

"Inuka, ushambulie Kedari
na kuwaangamiza watu wa
mashariki.
29 [j]Hema zao na makundi yao ya
kondoo yatachukuliwa;
vibanda vyao vitatwaliwa
pamoja na mali zao zote na
ngamia zao.
Watu watawapigia kelele,
'Hofu kuu iko kila upande!'

30 [k]"Kimbieni haraka!
Kaeni kwenye mapango marefu
sana, ninyi mkaao Hazori,"
asema BWANA.
"Nebukadneza, mfalme wa Babeli
amepanga shauri baya dhidi
yenu;
amebuni hila dhidi yenu.

---

[a]**49:20** Isa 14:27; Yer 50:45; Mao 1:10; Mal 1:3-4; Isa 34:5; Mwa 36:11
[b]**49:21** Za 114:7; Eze 31:16; Yer 51:29; Eze 26:18; Yer 50:46; Eze 26:15; 27:28
[c]21 Kwa Kiebrania ni Bahari ya Mafunjo.
[d]**49:22** Kum 28:49; Hab 1:8; Isa 13:8; Yer 48:40-41; 4:13; Hos 8:1; Nah 3:13; Mwa 36:33
[e]**49:23** 2Fal 14:28; Mdo 9:2; 1Fal 8:65; Eze 47:16; 2Fal 18:34; Mwa 49:4; Isa 57:20
[f]**49:24** Yer 13:21
[g]**49:26** Isa 17:12-14; Yer 50:30; Isa 9:17; 13:18
[h]**49:27** Eze 39:6; Amo 1:4; 1Fal 15:18; Yer 21:14; 43:12; Eze 39:6; Mwa 14:15
[i]**49:28** Mwa 25:13; Amu 6:3; Isa 21:13; Yer 10:22; Yos 11:1
[j]**49:29** Yer 6:25; 46:5; Za 120:5
[k]**49:30** Amu 6:2; Yos 11:1; Yer 10:22

31 [a]"Inuka na ulishambulie taifa lililo
starehe,
linaloishi kwa kujiamini,"
asema BWANA,
"taifa lisilo na malango wala
makomeo;
watu wake huishi peke yao.
32 [b]Ngamia wao watakuwa nyara,
nayo makundi yao makubwa ya
ng'ombe yatatekwa.
Wale walio maeneo ya mbali
nitawatawanya pande zote,
nami nitaleta maafa juu yao
kutoka kila upande,"
asema BWANA.
33 [c]"Hazori itakuwa makao ya mbweha,
mahali pa ukiwa milele.
Hakuna yeyote atakayeishi humo;
hakuna mtu atakayekaa ndani
yake."

*Ujumbe Kuhusu Elamu*

34 [d]Hili ndilo neno la BWANA lililomjia
nabii Yeremia kuhusu Elamu, mapema
katika utawala wa Sedekia mfalme wa
Yuda:

35 [e]Hili ndilo BWANA Mwenye Nguvu Zote
asemalo:

"Tazama, nitavunja upinde wa
Elamu,
ulio tegemeo la nguvu zao.
36 [f]Nitaleta pepo nne dhidi ya Elamu
toka pande nne za mbingu,
nitawatawanya katika hizo pande
nne,
wala hapatakuwa na taifa
ambalo watu wa Elamu
waliofukuzwa
hawatakwenda.
37 [g]Nitamfadhaisha Elamu mbele ya
adui zao,
mbele yao wale wanaotafuta uhai
wao;
nitaleta maafa juu yao,
naam, hasira yangu kali,"
asema BWANA.
"Nitawafuatia kwa upanga
mpaka nitakapowamaliza.
38 Nitaweka kiti changu cha enzi huko
Elamu
na kumwangamiza mfalme wake
na maafisa wake,"
asema BWANA.

39 [h]"Lakini nitarudisha mateka wa
Elamu
katika siku zijazo,"
asema BWANA.

*Ujumbe Kuhusu Babeli*

50 [i]Hili ndilo neno alilosema BWANA
kupitia nabii Yeremia kuhusu Babeli
na nchi ya Wakaldayo:

2 [j]"Tangazeni na mhubiri katikati ya
mataifa,
twekeni bendera na mkahubiri;
msiache kitu chochote, bali
semeni,
'Babeli utatekwa;
Beli ataaibishwa,
Merodaki atajazwa na hofu kuu.
Sanamu zake zitaaibishwa
na vinyago vyake vitajazwa hofu
kuu.'
3 [k]Taifa kutoka kaskazini
litamshambulia,
na kuifanya nchi yake ukiwa.
Hakuna hata mmoja atakayeishi
ndani yake,
watu na wanyama wataikimbia.

---

[a]**49:31** Eze 38:11; Hes 23:9; Mik 7:14
[b]**49:32** Yer 9:26; 25:22; Amu 6:5; Yer 13:24
[c]**49:33** Yer 10:22; 48:9; Isa 13:22; Hos 11:1
[d]**49:34** Mwa 10:22; 2Fal 24:18
[e]**49:35** Za 37:15; Ezr 4:9; Dan 8:2; Isa 22:6
[f]**49:36** Dan 11:4
[g]**49:37** Yer 44:2; 30:24; 9:16; Eze 32:24
[h]**49:39** Yer 48:47
[i]**50:1** Isa 13:1; Za 137:8; Mwa 10:10
[j]**50:2** Kum 30:4; Yer 4:16; 51:31, 47; Isa 21:9; Za 20:5; Isa 13:2; Yer 46:6; Law 26:30
[k]**50:3** Isa 14:22-23; Yer 9:11; Sef 1:3; Isa 13:17; 41:25; Yer 25:26

4 [a]“Katika siku hizo, wakati huo,”
asema BWANA,
“watu wa Israeli pamoja na watu wa
Yuda
wataenda wakilia ili kumtafuta
BWANA Mungu wao.
5 [b]Wataiuliza njia iendayo Sayuni
na kuelekeza nyuso zao huko.
Watakuja na kuambatana na BWANA
katika agano la milele
ambalo halitasahaulika.

6 [c]“Watu wangu wamekuwa kondoo
waliopotea;
wachungaji wao wamewapotosha
na kuwasababisha kuzurura
juu ya milima.
Walitangatanga juu ya mlima na
kilima,
na kusahau mahali pao wenyewe
pa kupumzikia.
7 [d]Yeyote aliyewakuta aliwala;
adui zao walisema, ‘Sisi hatuna
hatia,
kwa kuwa wao walitenda dhambi
dhidi ya BWANA, malisho yao
halisi,
BWANA, aliye tumaini la baba
zao.’

8 [e]“Kimbieni kutoka Babeli;
ondokeni katika nchi ya
Wakaldayo
tena kuweni kama mbuzi wale
waongozao kundi.
9 [f]Kwa maana nitaamsha na kuleta
dhidi ya Babeli
muungano wa mataifa makubwa
kutoka nchi ya kaskazini.
Watashika nafasi zao dhidi yake,
naye kutokea kaskazini atatekwa.
Mishale yao itakuwa kama mishale
ya mashujaa walio hodari,
ambao hawawezi kurudi mikono
mitupu.
10 Kwa hiyo Ukaldayo utatekwa nyara;
wote wamtekao nyara watapata za
kutosha,”
asema BWANA.

11 [g]“Kwa sababu hushangilia na
kufurahi,
wewe utekaye urithi wangu,
kwa sababu unachezacheza kama
mtamba anayepura nafaka,
na kulia kama farasi dume,
12 [h]mama yako ataaibika mno,
yeye aliyekuzaa atatahayari.
Atakuwa mdogo kuliko mataifa
mengine yote,
atakuwa nyika, nchi kame na
jangwa.
13 [i]Kwa sababu ya hasira ya BWANA
hatakaliwa na mtu,
lakini ataachwa ukiwa kabisa.
Wote watakaopita Babeli watatiwa
hofu na kudhihaki
kwa sababu ya majeraha yake
yote.

14 “Shikeni nafasi zenu kuzunguka
Babeli,
enyi nyote mvutao upinde.
Mpigeni! Msibakize mshale wowote,
kwa kuwa ametenda dhambi dhidi
ya BWANA.
15 [j]Piga kelele dhidi yake kila upande!
Anajisalimisha, minara yake
inaanguka,
kuta zake zimebomoka.
Kwa kuwa hiki ni kisasi cha BWANA,
mlipizeni kisasi;
mtendeeni kama alivyowatendea
wengine.

[a]**50:4** Eze 37:22; Ezr 3:12; Yer 31:9; Isa 9:13; Hos 3:5; Yer 3:18
[b]**50:5** 1Sam 29:1; Yer 33:7; Kum 29:14; Ebr 8:6-10; Isa 11:16; Yer 31:21; 32:40
[c]**50:6** Isa 53:6; Mt 10:6; Yer 3:6; Eze 34:6; Za 119:176; Mt 9:36; Yer 10:21; Za 95:10
[d]**50:7** Yer 2:3; 14:8; Za 22:4; Yer 5:17; 10:25; Eze 35:12
[e]**50:8** Isa 48:20; Ufu 18:4; Yer 51:6
[f]**50:9** Isa 13:17; Yer 25:14; Isa 41:25; Yer 25:26
[g]**50:11** Isa 47:6; Yer 31:18
[h]**50:12** Yer 51:47; 25:12; 51:26
[i]**50:13** Eze 27:36; Hab 2:6; Kum 29:22; Yer 49:17; 9:11; 48:9; 51:62; 18:16
[j]**50:15** Yer 51:14; 2Nya 30:8; Yer 51:44-58; 2Fal 25:4; Yer 51:6; Ufu 18:6; Isa 10:3; Hab 2:7-8

16 [a]Katilieni mbali mpanzi kutoka Babeli,
pamoja na mvunaji na mundu wake akivuna.
Kwa sababu ya upanga wa mdhalimu
kila mmoja na arejee kwa watu wake mwenyewe,
kila mmoja na akimbilie
kwenye nchi yake mwenyewe.

17 [b]"Israeli ni kundi lililotawanyika
ambalo simba wamelifukuzia mbali.
Wa kwanza kumla alikuwa mfalme wa Ashuru,
wa mwisho kuponda mifupa yake
alikuwa Nebukadneza mfalme wa Babeli."

18 [c]Kwa hiyo hili ndilo BWANA Mwenye Nguvu Zote, Mungu wa Israeli, asemalo:

"Nitamwadhibu mfalme wa Babeli na nchi yake
kama nilivyomwadhibu mfalme wa Ashuru.
19 [d]Lakini nitamrudisha Israeli katika malisho yake mwenyewe
naye atalisha huko Karmeli na Bashani;
njaa yake itashibishwa
juu ya vilima vya Efraimu na Gileadi.
20 [e]Katika siku hizo, wakati huo,"
asema BWANA,
"uchunguzi utafanyika kwa ajili ya kosa la Israeli,
lakini halitakuwepo,
kwa ajili ya dhambi za Yuda,
lakini haitapatikana hata moja,
kwa kuwa nitawasamehe
mabaki nitakaowaacha.

21 [f]"Shambulieni nchi ya Merathaimu
na wale waishio huko Pekodi.
Wafuatieni, waueni
na kuwaangamiza kabisa,"
asema BWANA.
"Fanyeni kila kitu nilichowaamuru.
22 [g]Kelele ya vita iko ndani ya nchi,
kelele ya maangamizi makuu!
23 [h]Tazama jinsi nyundo ya dunia yote
ilivyovunjika na kuharibika!
Tazama jinsi Babeli ilivyokuwa ukiwa
miongoni mwa mataifa!
24 [i]Nimetega mtego kwa ajili yako, ee Babeli,
nawe ukakamatwa kabla haujafahamu;
ulipatikana na ukakamatwa
kwa sababu ulimpinga BWANA.
25 [j]BWANA amefungua ghala lake la silaha
na kuzitoa silaha za ghadhabu yake,
kwa kuwa BWANA Mwenyezi Mwenye Nguvu Zote
anayo kazi ya kufanya
katika nchi ya Wakaldayo.
26 [k]Njooni dhidi yake kutoka mbali.
Zifungueni ghala zake za nafaka;
mlundikeni kama lundo la nafaka.
Mwangamizeni kabisa
na msimwachie mabaki yoyote.
27 [l]Waueni mafahali wake wachanga wote;
waacheni washuke machinjoni!
Ole wao! Kwa kuwa siku yao imewadia,
wakati wao wa kuadhibiwa.

---

[a]**50:16** Yer 25:38; Isa 13:14; Yer 51:9
[b]**50:17** 2Fal 24:1; Yer 2:15; Kum 4:27; 2Fal 17:6; 24:10-17; 1Pet 2:25; Yer 2:15; Hes 24:8
[c]**50:18** Isa 10:12; Eze 31:3; Sef 2:13
[d]**50:19** Yer 31:10; Eze 34:13; Yer 33:12; Isa 65:10; Mik 7:14; Zek 10:10
[e]**50:20** Za 103:12; Zek 3:4-9; Isa 33:24; Yer 31:34; Rum 9:27; Isa 10:20-22; Eze 36:16
[f]**50:21** Eze 23:23; Isa 10:6
[g]**50:22** Yer 4:19-21; 51:54
[h]**50:23** Isa 14:16; Yer 51:20; Isa 10:5
[i]**50:24** Yer 51:12; Dan 5:30-31; Yer 51:31; Ay 9:4
[j]**50:25** Isa 13:5
[k]**50:26** Isa 14:22-23; Yer 51:11; Rut 3:7
[l]**50:27** Za 68:30; Yer 48:15; Ay 18:20; Yer 25:34

28 [a]Wasikilizeni watoro na wakimbizi
kutoka Babeli
wakitangaza katika Sayuni
jinsi Bwana, Mungu wetu
alivyolipiza kisasi,
kisasi kwa ajili ya Hekalu lake.

29 [b]"Waiteni wapiga mishale dhidi ya
Babeli,
wote wale wavutao upinde.
Pigeni kambi kumzunguka kabisa,
asitoroke mtu yeyote.
Mlipizeni kwa matendo yake;
mtendeeni kama alivyotenda.
Kwa kuwa alimdharau Bwana,
yeye Aliye Mtakatifu wa Israeli.
30 [c]Kwa hiyo, vijana wake wanaume
wataanguka barabarani;
askari wake wote
watanyamazishwa siku ile,"
asema Bwana.
31 [d]"Tazama, niko kinyume nawe, ewe
mwenye majivuno,"
asema Bwana, Bwana Mwenye
Nguvu Zote,
"kwa kuwa siku yako imewadia,
yaani, wakati wako wa
kuadhibiwa.
32 [e]Mwenye majivuno atajikwaa na
kuanguka,
wala hakuna yeyote
atakayemuinua;
nitawasha moto katika miji yake,
utakaowateketeza wote
wanaomzunguka."

33 [f]Hili ndilo asemalo Bwana Mwenye Nguvu Zote:

"Watu wa Israeli wameonewa,
nao watu wa Yuda pia.
Wote waliowateka wamewashikilia
sana,
wanakataa kuwaachia waende.
34 [g]Lakini Mkombozi wao ana nguvu;
Bwana Mwenye Nguvu Zote ndilo
jina lake.
Atatetea kwa nguvu shauri lao
ili alete raha katika nchi yao,
lakini ataleta msukosuko
kwa wale waishio Babeli.

35 [h]"Upanga dhidi ya Wakaldayo!"
asema Bwana,
"dhidi ya wale waishio Babeli
na dhidi ya maafisa wake na watu
wenye busara!
36 Upanga dhidi ya manabii wake wa
uongo!
Watakuwa wapumbavu.
Upanga dhidi ya mashujaa wake!
Watajazwa na hofu kuu
37 [i]Upanga dhidi ya farasi na magari
yake ya vita
pamoja na askari wake wote wa
kigeni katika safu zake!
Wao watakuwa kama wanawake.
Upanga dhidi ya hazina zake!
Hizo zitatekwa nyara.
38 [j]Ukame juu ya maji yake!
Nayo yatakauka.
Kwa kuwa ni nchi ya sanamu,
wao wanaenda wazimu kwa ajili
ya sanamu.

39 [k]"Kwa hiyo, viumbe vya jangwani na
fisi wataishi humo,
nao bundi watakaa humo.
Kamwe haitakaliwa tena
wala watu hawataishi humo
kutoka kizazi hadi kizazi.

---

[a]**50:28** Isa 48:20; Yer 51:10; 2Fal 24:13; Yer 52:13
[b]**50:29** Ay 21:19; Ufu 18:6; Oba 1:15; Dan 5:23; Isa 14:13-14; Mao 3:24; Isa 13:18; Kum 32:41
[c]**50:30** Isa 13:18; Yer 49:26; 51:4
[d]**50:31** Yer 21:13; Ufu 18:7-8
[e]**50:32** Yer 21:14; 49:27; Amo 5:2; Za 20:8; 119:21
[f]**50:33** Isa 58:6; 14:17
[g]**50:34** Yer 31:35; 51:19; Za 119:154; Mao 3:58; Kut 6:6; Ay 19:25; Isa 49:25
[h]**50:35** Yer 47:6; Dan 5:7; Isa 37:13; 45:1
[i]**50:37** Yer 25:20; 2Fal 19:23; Isa 19:16; Yer 51:21; Nah 3:13; Isa 45:3
[j]**50:38** Isa 11:15; Yer 51:36; Ufu 16:12
[k]**50:39** Isa 34:13-15; Ufu 18:2; Isa 13:19-22; Za 74:14; Yer 51:37

40 [a]Kama vile Mungu alivyoangamiza
Sodoma na Gomora
pamoja na miji iliyokuwa jirani
nayo,"
asema BWANA,
"vivyo hivyo hakuna mtu yeyote
atakayeishi humo.
Naam, hakuna mtu yeyote
atakayekaa humo.

41 [b]"Tazama! Jeshi linakuja kutoka
kaskazini;
taifa kubwa na wafalme wengi
wanaamshwa kutoka miisho ya
dunia.
42 [c]Wamejifunga pinde na mikuki;
ni wakatili na wasio na huruma.
Wanatoa sauti kama bahari
inayonguruma
wanapoendesha farasi zao;
wanakuja kama watu waliojipanga
tayari kwa vita
ili kukushambulia, ee Binti Babeli.
43 [d]Mfalme wa Babeli amesikia habari
kuwahusu,
nayo mikono yake imelegea.
Uchungu umemshika,
maumivu kama ya mwanamke
katika utungu wa kuzaa.
44 [e]Kama simba anayepanda kutoka
vichaka vya Yordani
kuja kwenye nchi ya malisho
mengi,
ndivyo nitamfukuza Babeli kutoka
nchi yake ghafula.
Ni nani aliye mteule,
nitakayemweka kwa ajili ya jambo
hili?
Ni nani aliye kama mimi,
na ni nani awezaye kunipinga?
Tena ni mchungaji yupi
awezaye kusimama kinyume
nami?"
45 [f]Kwa hiyo, sikia kile BWANA
alichokipanga dhidi ya Babeli,
kile alichokusudia dhidi ya nchi ya
Wakaldayo:
Aliye mchanga katika kundi
ataburutwa mbali.
Yeye ataharibu kabisa malisho yao
kwa sababu yao.
46 [g]Kwa sauti ya kutekwa kwa Babeli,
dunia itatetemeka;
kilio chake kitasikika pote
miongoni mwa mataifa.

51 [hi]Hili ndilo asemalo BWANA:
"Tazama nitaamsha
roho ya mwangamizi
dhidi ya Babeli na watu wakaao
Leb-Kamai.[j]
2 Nitawatuma wageni Babeli
kumpepeta na kuiharibu nchi
yake;
watampinga kila upande
katika siku ya maafa yake.
3 [k]Usimwache mpiga upinde afunge
kamba upinde wake,
wala usimwache avae silaha zake.
Usiwaonee huruma vijana wake;
angamiza jeshi lake kabisa.
4 [l]Wataanguka waliouawa katika
Babeli,
wakiwa na majeraha ya kutisha
barabarani zake.

[a]**50:40** Mwa 19:24; Mt 10:15; 2Pet 2:6; Yer 51:62
[b]**50:41** Isa 41:25; Yer 6:22; Isa 13:14; Yer 51:22-28; Ufu 17:16; Isa 23:17
[c]**50:42** Isa 13:18; 5:30; 47:1; Yer 6:23; Ay 30:21
[d]**50:43** Yer 47:3; 6:22-24
[e]**50:44** Hes 16:5; Ay 41:10; Isa 46:9; Yer 12:5; 49:19
[f]**50:45** Isa 24:14; Mdo 4:28; Isa 48:14; Yer 51:11
[g]**50:46** Ay 24:12; Ufu 18:9-10; Amu 5:4; Yer 49:21
[h]**51:1** Isa 41:16; Mt 3:12; Yer 50:14; Isa 13:5-9
[i]**51:1** Yer 46:4; Isa 41:25; Yer 50:28, 45; Isa 13:3; Yer 50:9; Isa 21:5; 41:2
[j]1 Leb-Kamai ni Ukaldayo, yaani Babeli, kwa fumbo.
[k]**51:3** Yer 50:29; 46:4
[l]**51:4** Isa 13:15-18; Yer 50:30

5 [a]Kwa maana Israeli na Yuda
hawajaachwa
na Mungu wao, BWANA Mwenye
Nguvu Zote,
ingawa nchi yao imejaa uovu
mbele zake yeye Aliye Mtakatifu
wa Israeli.

6 [b]"Kimbieni kutoka Babeli!
Okoeni maisha yenu!
Msiangamizwe kwa sababu ya
dhambi zake.
Ni wakati wa kisasi cha BWANA,
atamlipa kile anachostahili.
7 [c]Babeli alikuwa kikombe cha
dhahabu katika mkono wa
BWANA;
aliufanya ulimwengu wote ulewe.
Mataifa walikunywa mvinyo wake;
kwa hiyo sasa wameingiwa na
wazimu.
8 [d]Babeli ataanguka ghafula na
kuvunjika.
Mwombolezeni!
Tafuteni zeri ya kutuliza maumivu
yake,
labda anaweza kupona.

9 [e]" 'Tungemponya Babeli,
lakini hawezi kuponyeka;
tumwacheni, na kila mmoja wetu
aende nchi yake mwenyewe,
kwa kuwa hukumu yake inafika
angani,
inapanda juu hadi mawinguni.'

10 [f]" 'BWANA amethibitisha haki yetu;
njooni, tutangaze katika Sayuni
kitu ambacho BWANA Mungu
wetu amefanya.'

11 "Noeni mishale,
chukueni ngao!
BWANA amewaamsha wafalme wa
Wamedi,
kwa sababu nia yake ni
kuangamiza Babeli.
BWANA atalipiza kisasi,
kisasi kwa ajili ya Hekalu lake.
12 [g]Twekeni bendera juu ya kuta za
Babeli!
Imarisheni ulinzi,
wekeni walinzi,
andaeni waviziao!
BWANA atatimiza kusudi lake,
amri yake juu ya watu wa Babeli.
13 [h]Wewe uishiye kando ya maji mengi
na uliye na wingi wa hazina,
mwisho wako umekuja,
wakati wako wa kukatiliwa mbali.
14 [i]BWANA Mwenye Nguvu Zote
ameapa kwa nafsi yake
mwenyewe:
'Hakika nitakujaza na watu, kama
kundi la nzige,
nao watapiga kelele za ushindi juu
yako.'

15 [j]"Aliiumba dunia kwa uweza wake;
akaweka misingi ya ulimwengu
kwa hekima yake
na akazitandaza mbingu kwa
ufahamu wake.
16 [k]Atoapo sauti yake, maji yaliyo
katika mbingu hunguruma,
huyafanya mawingu yainuke
kutoka miisho ya dunia.
Hupeleka umeme wa radi pamoja na
mvua,
naye huuleta upepo kutoka ghala
zake.

---

[a]**51:5** Law 26:44; Isa 54:6-8; Za 91:14; Hos 4:1
[b]**51:6** Ufu 18:4; Isa 48:20; Yer 50:8, 15; Ay 21:19; Isa 1:24; Mao 3:64; Hes 16:26
[c]**51:7** Isa 51:22; Ufu 17:4; Yer 25:15-16; 49:12; Ufu 14:8-10
[d]**51:8** Isa 14:15; Ufu 14:8; Yer 8:22; Ufu 18:9; Yer 46:11; Isa 21:9
[e]**51:9** Isa 13:14; 31:9; Ufu 18:4-5; Yer 50:16
[f]**51:10** Mik 7:8-9; Za 64:9; Yer 50:28
[g]**51:12** Za 20:5; 2Sam 18:24; Eze 33:2
[h]**51:13** Yer 50:38; Ufu 17:15; Eze 22:27; Hab 2:9; Isa 45:3
[i]**51:14** Mwa 22:16; Amo 6:8; Nah 3:15; Yer 50:15
[j]**51:15** Ay 9:8; Isa 40:26; Mdo 14:15; Za 104:24; 136:5
[k]**51:16** Za 18:11-13; Kum 28:12; Yn 1:12; Ay 28:26; Za 135:7

17 [a]“Kila mtu ni mjinga na hana
maarifa;
kila sonara ameaibishwa na
sanamu zake.
Vinyago vyake ni vya udanganyifu,
havina pumzi ndani yavyo.
18 [b]Havifai kitu, ni vitu vya kufanyia
mzaha,
hukumu yavyo itakapowadia,
vitaangamia.
19 [c]Yeye Aliye Fungu la Yakobo sivyo
alivyo,
kwani ndiye Muumba wa vitu
vyote,
pamoja na kabila la urithi wake:
Bwana Mwenye Nguvu Zote ndilo
jina lake.

20 [d]“Wewe ndiwe rungu langu la vita,
silaha yangu ya vita:
kwa wewe navunjavunja mataifa,
kwa wewe naangamiza falme,
21 [e]kwa wewe navunjavunja
farasi na mpanda farasi,
kwa wewe navunjavunja
gari la vita na mwendeshaji wake,
22 [f]kwa wewe napondaponda
mwanaume na mwanamke,
kwa wewe napondaponda
mzee na kijana,
kwa wewe napondaponda
kijana wa kiume na mwanamwali,
23 kwa wewe nampondaponda
mchungaji na kundi,
kwa wewe nampondaponda
mkulima na maksai,
kwa wewe nawapondaponda
watawala na maafisa.

24 [g]“Mbele ya macho yako nitamlipiza
Babeli na wote waishio Ukaldayo kwa ajili
ya makosa yote waliyofanya katika Sayuni,”
asema Bwana.

25 [h]“Mimi niko kinyume nawe, ee
mlima unaoharibu,
wewe uangamizaye dunia yote,”
asema Bwana.
“Nitanyoosha mkono wangu dhidi
yako,
nikuvingirishe kutoka kwenye
kilele cha mwamba,
na kukufanya mlima ulioteketezwa
kwa moto.
26 [i]Hakuna jiwe litakalochukuliwa
kutoka kwako
kwa ajili ya kufanywa jiwe la
pembeni,
wala jiwe lolote kwa ajili ya msingi,
kwa maana utakuwa ukiwa
milele,”
asema Bwana.

27 [j]“Twekeni bendera katika nchi!
Pigeni tarumbeta katikati ya
mataifa!
Andaeni mataifa kwa ajili ya vita
dhidi yake,
iteni falme hizi dhidi yake:
Ararati, Mini na Ashkenazi.
Wekeni jemadari dhidi yake,
pelekeni farasi wengi kama kundi
la nzige.
28 Andaeni mataifa kwa ajili ya vita
dhidi yake,
wafalme wa Wamedi,
watawala wao na maafisa wao wote,
pamoja na nchi zote
wanazotawala.
29 [k]Nchi inatetemeka na kugaagaa,
kwa kuwa makusudi ya Bwana
dhidi ya Babeli yanasimama:
yaani, kuangamiza nchi ya Babeli
ili pasiwe na yeyote atakayeishi
humo.

---

[a]**51:17** Isa 44:20; Hab 2:18-19; Yer 50:2
[b]**51:18** Yer 18; 15; Yn 2:8
[c]**51:19** Za 119:57; Kut 34:9
[d]**51:20** Isa 10:5; Zek 9:13; Mik 4:13; Ay 34:24; Isa 45:1
[e]**51:21** Kut 15:1; Isa 43:17; Yer 50:37
[f]**51:22** 2Nya 36:17; Isa 13:17-18
[g]**51:24** Kum 32:41; Mao 3:64; Yer 50:15; Isa 45:1
[h]**51:25** Yer 21:13; 50:23; Kut 3:20; Zek 4:7
[i]**51:26** Isa 13:19-22; Yer 50:12
[j]**51:27** Isa 13:2; Za 20:5; Mwa 8:4; 10:3; Yer 25:14
[k]**51:29** Isa 13:20; Yer 50:13; Amu 5:4; Yer 49:21; Za 33:11; Yer 48:9

30 [a]Mashujaa wa Babeli wameacha
kupigana,
wamebaki katika ngome zao.
Nguvu zao zimekwisha,
wamekuwa kama wanawake.
Makazi yake yameteketezwa kwa
moto,
makomeo ya malango yake
yamevunjika.
31 [b]Tarishi mmoja humfuata mwingine,
na mjumbe humfuata mjumbe,
kumtangazia mfalme wa Babeli
kwamba mji wake wote
umetekwa,
32 [c]Vivuko vya mito vimekamatwa,
mabwawa yenye mafunjo
yametiwa moto,
nao askari wameingiwa na hofu
kuu."

33 [d]Hili ndilo BWANA Mwenye Nguvu Zote, Mungu wa Israeli, asemalo:

"Binti Babeli ni kama sakafu ya
kupuria
wakati inapokanyagwa;
wakati wa kumvuna utakuja
upesi."

34 [e]"Nebukadneza mfalme wa Babeli
ametula,
ametufanya tuchangayikiwe,
ametufanya tuwe gudulia tupu.
Kama nyoka ametumeza
na kujaza tumbo lake kwa vyakula
vyetu vizuri,
kisha akatutapika.
35 Jeuri iliyofanyiwa miili yetu[f] na iwe
juu ya Babeli,"
ndivyo wasemavyo wakaao
Sayuni.
"Damu yetu na iwe juu ya wale
waishio Babeli,"
asema Yerusalemu.

36 [g]Kwa hiyo, hili ndilo BWANA asemalo:

"Tazama, nitatetea shauri lako
na kulipiza kisasi kwa ajili yako;
nitaikausha bahari yake
na kuzikausha chemchemi zake.
37 [h]Babeli utakuwa lundo la magofu
na makao ya mbweha,
kitu cha kutisha na kudharauliwa,
mahali asipoishi mtu.
38 Watu wake wote wananguruma
kama simba wadogo,
wanakoroma kama wana simba.
39 [i]Lakini wakati wakiwa
wameamshwa,
nitawaandalia karamu
na kuwafanya walewe,
ili wapige kelele kwa kicheko,
kisha walale milele na wasiamke,"
asema BWANA.
40 "Nitawateremsha kama wana-
kondoo waendao machinjoni,
kama kondoo dume na mbuzi.

41 [j]"Tazama jinsi Sheshaki[k]
atakamatwa,
majivuno ya dunia yote
yatakavyonyakuliwa.
Babeli atakuwa mwenye hofu kiasi
gani
kati ya mataifa!
42 [l]Bahari itainuka juu ya Babeli;
mawimbi yake yenye kunguruma
yatamfunika.
43 [m]Miji yake itakuwa ukiwa,
kame na jangwa,

---

[a]**51:30** Yer 50:24; 2Sam 19:16; Mao 2:9; Nah 3:13; Isa 47:14; 45:2
[b]**51:31** Yer 50:24; 2Sam 18:19-31; Dan 5:30
[c]**51:32** Isa 47:14; Yer 50:36
[d]**51:33** Isa 21:10; 17:5; Hos 6:11; Mt 13:30; Isa 13:22
[e]**51:34** Yer 50:17; Nah 2:12; Hos 8:8
[f]35 Au: Jeuri tuliyofanyiwa sisi na watoto wetu.
[g]**51:36** Za 140:12; Mao 3:58; Yer 20:12; Rum 12:19; Hos 13:15; Yer 50:34; Isa 11:15
[h]**51:37** Isa 13:22; Ufu 12:8; Yer 50:39; 18:16; Ufu 18:2; Nah 3:6; Mal 2:9
[i]**51:39** Isa 21:5; Yer 50:24; Za 13:3
[j]**51:41** Yer 25:26; Isa 13:19; Dan 4:30; Yer 50:13
[k]41 Sheshaki ni Babeli kwa fumbo.
[l]**51:42** Za 18:4; Isa 8:7-8
[m]**51:43** Isa 13:20; Yer 2:6; Isa 21:1

nchi ambayo hakuna yeyote
anayeishi ndani yake,
ambayo hakuna mtu anayepita
humo.
44 [a]Nitamwadhibu Beli katika Babeli,
na kumfanya atapike kile
alichokimeza.
Mataifa hayatamiminika tena kwake.
Nao ukuta wa Babeli utaanguka.

45 [b]“Tokeni ndani yake, enyi watu
wangu!
Okoeni maisha yenu!
Ikimbieni hasira kali ya BWANA.
46 [c]Msikate tamaa wala msiogope tetesi
zitakaposikika katika nchi;
tetesi moja inasikika mwaka huu,
nyingine mwaka unaofuata;
tetesi juu ya jeuri katika nchi,
na ya mtawala dhidi ya mtawala.
47 [d]Kwa kuwa hakika wakati utawadia
nitakapoziadhibu sanamu za
Babeli;
nchi yake yote itatiwa aibu,
na watu wake wote waliouawa
wataangukia ndani yake.
48 [e]Ndipo mbingu na dunia na vyote
vilivyomo ndani yake
vitapiga kelele za shangwe juu ya
Babeli,
kwa kuwa kutoka kaskazini
waharabu watamshambulia,”
asema BWANA.

49 [f]“Babeli ni lazima aanguke kwa
sababu ya kuwaua Waisraeli,
kama vile waliouawa duniani kote
walivyoanguka kwa sababu ya
Babeli.
50 Wewe uliyepona upanga,
ondoka wala usikawie!
Mkumbuke BWANA ukiwa katika
nchi ya mbali,
na utafakari juu ya Yerusalemu.”

51 [g]“Tumetahayari, kwa maana
tumetukanwa
na aibu imefunika nyuso zetu,
kwa sababu wageni wameingia
mahali patakatifu pa nyumba ya
BWANA.”

52 [h]“Lakini siku zinakuja,” asema
BWANA,
“nitakapoadhibu sanamu zake,
na katika nchi yake yote
waliojeruhiwa watalia kwa
maumivu makali.
53 [i]Hata kama Babeli ikifika angani
na kuziimarisha ngome zake
ndefu,
nitatuma waharabu dhidi yake,”
asema BWANA.

54 “Sauti ya kilio inasikika kutoka
Babeli,
sauti ya uharibifu mkuu
kutoka nchi ya Wakaldayo.
55 [j]BWANA ataiangamiza Babeli,
atanyamazisha makelele ya
kishindo chake.
Mawimbi ya adui yatanguruma
kama maji makuu,
ngurumo ya sauti zao itavuma.
56 [k]Mharabu atakuja dhidi ya Babeli,
mashujaa wake watakamatwa,
nazo pinde zao zitavunjwa.
Kwa kuwa BWANA ni Mungu wa
kisasi,
yeye atalipiza kikamilifu.
57 [l]Nitawafanya maafisa wake na
wenye busara walewe,
watawala wao, maafisa, pamoja na
wapiganaji wao;

[a]**51:44** Isa 21:9; 2Fal 25:4; Isa 25:12; 46:1; Yer 50:15
[b]**51:45** Ufu 18:4; Yer 50:8; Isa 48:20; Za 76:10; 79:6
[c]**51:46** Yer 46:27; 2Fal 19:7; Za 18:45
[d]**51:47** Isa 46:1-2; Yer 50:12; 27:7; 50:12
[e]**51:48** Isa 44:23; Ufu 18:20; Yer 25:26; Isa 41:25; Za 149:2; Ay 3:7
[f]**51:49** Za 137:8; Yer 50:29
[g]**51:51** Za 44:13-16; 79:4; Mao 1:10
[h]**51:52** Ay 24:12
[i]**51:53** Mwa 11:4; Isa 14:13-14; Ay 15:21; Yer 49:16
[j]**51:55** Za 18:4; Isa 25:5
[k]**51:56** Ay 15:21; Mwa 4:24; Za 46:9; Hab 2:8; Za 94:1-2
[l]**51:57** Za 76:5; Yer 25:27; Isa 6:5; Yer 46:18; Ay 5:13; Isa 21:7

watalala milele na hawataamka,”
asema Mfalme, ambaye jina lake
ni BWANA Mwenye Nguvu
Zote.

58 [a]Hili ndilo BWANA Mwenye Nguvu
Zote asemalo:

“Ukuta mnene wa Babeli
utasawazishwa,
na malango yaliyoinuka
yatateketezwa kwa moto;
mataifa yanajichosha bure,
taabu ya mataifa ni nishati tu ya
miali ya moto.”

59 [b]Huu ndio ujumbe Yeremia aliompa
afisa Seraya mwana wa Neria mwana wa
Maaseya, alipokwenda Babeli pamoja na
Sedekia mfalme wa Yuda, katika mwaka
wa nne wa utawala wake. 60 [c]Yeremia
alikuwa ameandika ndani ya kitabu kuhusu
maafa yote yatakayoipata Babeli, yaani
yote yaliyokuwa yameandikwa kuhusu
Babeli. 61 Yeremia akamwambia Seraya,
“Utakapofika Babeli, hakikisha kwamba
umesoma maneno haya yote kwa sauti
kubwa. 62 [d]Kisha sema, ‘Ee BWANA, umesema
utaangamiza mahali hapa ili mtu wala
mnyama asiishi ndani yake, napo patakuwa
ukiwa milele.’ 63 [e]Utakapomaliza kusoma
hiki kitabu, kifungie jiwe kisha ukitupe
ndani ya Mto Frati. 64 [f]Kisha sema, ‘Hivi
ndivyo Babeli utakavyozama na usiinuke
tena, kwa sababu ya maafa nitakayoleta
juu yake. Nao watu wake wataanguka.’ ”

Maneno ya Yeremia yanaishia hapa.

*Anguko La Yerusalemu*

**(2 Wafalme 24:18–25:30)**

52 [g]Sedekia alikuwa na umri wa miaka
ishirini na mmoja alipoanza kutawala,
naye akatawala huko Yerusalemu kwa
miaka kumi na mmoja. Jina la mama yake
aliitwa Hamutali binti Yeremia, kutoka
Libna. 2 [h]Alifanya maovu machoni pa
BWANA, kama alivyofanya Yehoyakimu.
3 [i]Ilikuwa ni kwa sababu ya hasira ya
BWANA haya yote yalitokea Yerusalemu na
Yuda, naye mwishoni akawaondoa mbele
zake.

Basi, Sedekia akaasi dhidi ya mfalme wa
Babeli.

4 [j]Hivyo katika mwaka wa tisa wa
utawala wa Sedekia, katika siku ya kumi
ya mwezi wa kumi, Nebukadneza mfalme
wa Babeli akiwa na jeshi lake lote alifanya
vita dhidi ya Yerusalemu. Wakapiga kambi
nje ya mji na kuuzunguka mji pande zote.
5 Mji ulizungukwa na jeshi mpaka mwaka
wa kumi na moja wa utawala wa Mfalme
Sedekia.

6 [k]Ilipowadia siku ya tisa ya mwezi wa
nne, njaa ikazidi kuwa kali sana ndani ya
mji, hadi hapakuwa na chakula kwa ajili
ya watu. 7 [l]Kisha ukuta wa mji ukavunjwa
na jeshi lote likakimbia. Wakaondoka mjini
usiku kupitia lango lililokuwa kati ya kuta
mbili karibu na bustani ya mfalme, ingawa
Wakaldayo walikuwa wameuzunguka mji.
Wakakimbia kuelekea Araba. 8 Lakini jeshi
la Wakaldayo likamfuatia Mfalme Sedekia
na kumpata katika sehemu tambarare za
Yeriko. Askari wake wote wakatengwa naye
na kutawanyika, 9 [m]naye akakamatwa.

Akapelekwa kwa mfalme wa Babeli huko
Ribla, katika nchi ya Hamathi, mahali
ambapo alimtangazia hukumu. 10 [n]Huko
Ribla mfalme wa Babeli aliwachinja wana
wa Sedekia mbele ya macho yake. Pia
akawaua maafisa wote wa Yuda. 11 [o]Kisha
akayang’oa macho ya Sedekia, akamfunga
kwa pingu za shaba na kumpeleka Babeli,

---

[a]**51:58** 2Fal 25:4; Isa 15:4; 47:14; Hab 2:13; Isa 13:2
[b]**51:59** Yer 36:4; 52:1; 28:1
[c]**51:60** Kut 17:14; Yer 30:2; 36:2
[d]**51:62** Isa 13:20; Yer 9:11; 50:13
[e]**51:63** Mwa 2:14
[f]**51:64** Ay 31:40; Za 18:21; Eze 26:21; 28:19
[g]**52:1** 2Fal 24:17-18; Yos 10:29; Hes 33:20; 2Fal 8:22
[h]**52:2** Yer 36:30
[i]**52:3** Eze 17:12-16; Kut 33:15; Mwa 4:14
[j]**52:4** Zek 8:19; 2Fal 25:1-7; Yer 34:1; Eze 24:1-2; Kum 28:52-57
[k]**52:6** Law 26:26; Mao 1:11; Eze 4:16
[l]**52:7** Mao 4:19
[m]**52:9** Yer 21:7; 32:4; Hes 34:11; 13:21
[n]**52:10** Yer 22:30; 39:6-7
[o]**52:11** Eze 12:13; 17:16; Yer 34:4

alipomweka gerezani mpaka siku ya kifo
chake.
12 [a]Mnamo siku ya kumi ya mwezi wa
tano, katika mwaka wa kumi na tisa
wa utawala wa Nebukadneza mfalme
wa Babeli, Nebuzaradani jemadari wa
askari walinzi wa mfalme, aliyemtumikia
mfalme wa Babeli, alikuja Yerusalemu.
13 [b]Alichoma moto Hekalu la BWANA, jumba
la kifalme, na nyumba zote za Yerusalemu.
Aliteketeza kila jengo muhimu. 14 Jeshi
lote la Wakaldayo chini ya jemadari wa
askari walinzi wa mfalme walivunja
kuta zote zilizoizunguka Yerusalemu.
15 [c]Nebuzaradani, jemadari wa askari
walinzi, akawapeleka uhamishoni baadhi
ya watu maskini sana na wale waliobaki
katika mji, pamoja na mabaki ya watu wa
kawaida, na wale waliojisalimisha kwa
mfalme wa Babeli. 16 Lakini Nebuzaradani
akawaacha mabaki ya wale watu maskini
kabisa ili watunze mashamba ya mizabibu
na mashamba mengine.
17 [d]Wakaldayo walivunja vipande
zile nguzo za shaba, vile vishikilio vya
shaba vilivyohamishika, na ile Bahari ya
shaba, ambavyo vyote vilikuwa katika
Hekalu la BWANA. Hivyo wakaichukua
hiyo shaba yote na kuipeleka Babeli.
18 [e]Wakachukua pia vyungu, masepetu,
mikasi ya kusawazishia tambi, mabakuli
ya kunyunyizia, sahani na vyombo vyote
vya shaba vilivyotumika katika huduma
ya Hekalu. 19 [f]Jemadari wa askari walinzi
wa mfalme akachukua yale masinia, vile
vyetezo, yale mabakuli ya kunyunyizia, zile
sufuria, vile vinara vya taa, zile sahani na
yale mabakuli yaliyotumika kwa sadaka
za vinywaji, vitu vyote vile vilivyokuwa
vimetengenezwa kwa dhahabu safi au
fedha.
20 [g]Shaba iliyotokana na zile nguzo mbili,
ile Bahari na wale mafahali kumi na mawili
wa shaba waliokuwa chini yake, pamoja na
vile vishikilio vilivyohamishika, ambavyo
Mfalme Solomoni alikuwa ametengeneza
kwa ajili ya Hekalu la BWANA, ilikuwa na
uzito usioweza kupimika. 21 Kila nguzo
ilikuwa na urefu wa dhiraa kumi na nane,
kimo chake na mzunguko dhiraa kumi na
mbili, na unene wa nyanda nne, na zote
zilikuwa wazi ndani. 22 [h]Sehemu ya shaba
juu ya ile nguzo moja ilikuwa na urefu
wa dhiraa tano, na ilikuwa imepambwa
kwa wavu na makomamanga ya shaba
kuizunguka kote. Ile nguzo nyingine
pamoja na makomamanga yake ilifanana
na hiyo ya kwanza. 23 Kulikuwa na
makomamanga tisini na sita pembeni; jumla
ya makomamanga juu ya wavu uliokuwa
umezunguka yalikuwa mia moja.
24 [i]Yule jemadari wa askari walinzi
akawachukua kama wafungwa Seraya
kuhani mkuu, kuhani Sefania aliyefuata kwa
cheo, na mabawabu watatu. 25 [j]Miongoni
mwa wale watu waliokuwa wamesalia
katika mji, alimchukua afisa kiongozi wa
wapiganaji, na washauri saba wa mfalme.
Akamchukua pia mwandishi aliyesimamia
uandikishaji wa watu wa nchi, pamoja na
watu wake sitini waliopatikana ndani ya mji.
26 Nebuzaradani jemadari akawachukua hao
wote na kuwapeleka kwa mfalme wa Babeli
huko Ribla. 27 [k]Huko Ribla, katika nchi ya
Hamathi, mfalme wa Babeli akaamuru
wanyongwe.
Hivyo Yuda wakaenda utumwani, mbali
na nchi yao. 28 [l]Hii ndiyo hesabu ya watu
ambao Nebukadneza aliwachukua kwenda
uhamishoni:

katika mwaka wa saba,
  Wayahudi 3,023;
29 katika mwaka wa kumi na nane wa
  utawala wa Nebukadneza,

[a]**52:12** Zek 8:19; Yer 39:9; Zek 7:5
[b]**52:13** 2Nya 36:19; Kum 29:24; Mik 3:12; Za 74:8; Yer 19:13; Kum 13:16; Mao 2:6
[c]**52:15** 2Fal 24:1; Yer 38:19; 1:3
[d]**52:17** 1Fal 7:15, 27-37; Yer 27:19-22
[e]**52:18** Kut 27:3; 1Fal 7:45; Hes 4:14
[f]**52:19** Law 10:1; 1Fal 7:50; Hes 3:31; Kut 25:29; Hes 4:7; Dan 5:2; Ezr 1:7
[g]**52:20** 1Fal 7:25, 47
[h]**52:22** 1Fal 7:15-16, 20, 47; Kut 28:33
[i]**52:24** 2Fal 25:18; Yer 37:3; 21:1; 2Fal 12:9
[j]**52:25** Yer 36:10
[k]**52:27** Yer 20:4; Law 26:33; Hes 34:11
[l]**52:28** 2Fal 24:14-16; Neh 1:2; 2Nya 36:20; Kum 28:36

watu 832 kutoka Yerusalemu;
30 [a]katika mwaka wa ishirini na tatu
wa utawala wake,
Wayahudi 745 walichukuliwa
kwenda uhamishoni na
Nebuzaradani jemadari wa askari
walinzi wa mfalme.
Jumla ya watu wote walikuwa
4,600.

*Yehoyakini Anaachiwa Huru*

31 [b]Katika mwaka wa thelathini na
saba tangu Yehoyakini mfalme wa Yuda
apelekwe uhamishoni, katika mwaka ule
ambao Evil-Merodaki[c] alifanyika mfalme
wa Babeli, alimwacha huru Yehoyakini
mfalme wa Yuda, na kumfungua kutoka
gerezani siku ya ishirini na tano ya mwezi
wa kumi na mbili.
32 Alizungumza naye
kwa upole na kumpa kiti cha heshima zaidi
kuliko wale wafalme wengine aliokuwa nao
huko Babeli.
33 [d]Hivyo Yehoyakini akayavua
mavazi yake ya mfungwa, na siku zote za
maisha yake zilizobaki alikula mezani
mwa mfalme.
34 [e]Siku kwa siku mfalme wa
Babeli alimpa Yehoyakini posho siku zote
za maisha yake, hadi siku ya kifo chake.

---

[a]**52:30** Yer 43:3; 13:19
[b]**52:31** 2Fal 25:27-30; Mwa 40:13-20
[c]31 Pia aliitwa Ameli-Mariduki.
[d]**52:33** 2Sam 9:7, 13
[e]**52:34** 2Sam 9:10

# MAOMBOLEZO

1 [a] [b]Tazama jinsi mji ulivyoachwa
ukiwa,
mji ambao zamani ulikuwa umejaa
watu!
Jinsi ambavyo umekuwa kama
mama mjane,
ambaye wakati fulani alikuwa
maarufu miongoni mwa
mataifa!
Yule ambaye alikuwa malkia
miongoni mwa majimbo
sasa amekuwa mtumwa.

2 [c]Kwa uchungu, hulia sana usiku,
machozi yapo kwenye mashavu
yake.
Miongoni mwa wapenzi wake wote
hakuna yeyote wa kumfariji.
Rafiki zake wote wamemsaliti,
wamekuwa adui zake.

3 [d]Baada ya mateso na kufanyishwa
kazi kikatili,
Yuda amekwenda uhamishoni.
Anakaa miongoni mwa mataifa,
hapati mahali pa kupumzika.
Wote ambao wanamsaka
wamemkamata
katikati ya dhiki yake.

4 [e]Barabara zielekeazo Sayuni
zaomboleza,
kwa kuwa hakuna yeyote
anayekuja
kwenye sikukuu zake
zilizoamriwa.
Malango yake yote yamekuwa
ukiwa,
makuhani wake wanalia kwa
uchungu,
wanawali wake wanahuzunika,
naye yuko katika uchungu wa
maumivu makuu.

5 [f]Adui zake wamekuwa mabwana
zake,
watesi wake wana raha.
Bwana amemletea huzuni
kwa sababu ya dhambi zake
nyingi.
Watoto wake wamekwenda
uhamishoni,
mateka mbele ya adui.

6 [g]Fahari yote imeondoka
kutoka kwa Binti Sayuni.
Wakuu wake wako kama ayala
ambaye hapati malisho,
katika udhaifu wamekimbia
mbele ya anayewasaka.

7 [h]Katika siku za mateso yake na
kutangatanga,
Yerusalemu hukumbuka hazina
zote
ambazo zilikuwa zake siku za kale.
Wakati watu wake walipoanguka
katika mikono ya adui,
hapakuwepo na yeyote wa
kumsaidia.
Watesi wake walimtazama
na kumcheka katika maangamizi
yake.

8 [i]Yerusalemu ametenda dhambi sana
kwa hiyo amekuwa najisi.
Wote waliomheshimu wanamdharau,
kwa maana wameuona uchi wake.

---

[a]Sura hii imetungwa kila beti likianzia, na pia kila mstari katika lile beti, na herufi ya alfabeti ya Kiebrania zikifuatana tangu Aleph (A) hadi Taw (T); zote ni 22.
[b]**1:1** Isa 47:7-8; Ezr 4:20; Eze 5:5; Isa 3:26; Yer 42:2; Law 26:43; Mao 1:9
[c]**1:2** Za 6:6; Yer 4:30; Mik 7:5; Yer 30:14; 13:17; Mao 1:16; Ay 7:3
[d]**1:3** Yer 13:19; Kum 28:64-65; Kut 15:9; Law 26:14, 32, 33
[e]**1:4** Isa 27:10; Yer 9:11; Yoe 1:8-13
[f]**1:5** Isa 22:5; Yer 10:20; 39:9; 30:14; Mao 3:39; Yer 30:15; 52:28-30; Za 5:10; Mao 2:17
[g]**1:6** Yer 13:18; Za 9:14; Law 26:36
[h]**1:7** 2Fal 14:26; Yer 37:7; Mik 4:11; Mao 4:17; Yer 2:26
[i]**1:8** Isa 59:2-13; Za 38:8; Yer 13:22-26; 2:22

Yeye mwenyewe anapiga kite
na kugeukia mbali.

9 [a]Uchafu wake umegandamana na nguo zake;
hakuwaza juu ya maisha yake ya baadaye.
Anguko lake lilikuwa la kushangaza,
hapakuwepo na yeyote wa kumfariji.
"Tazama, Ee BWANA, teso langu,
kwa maana adui ameshinda."

10 [b]Adui ametia mikono
juu ya hazina zake zote,
aliona mataifa ya kipagani
wakiingia mahali patakatifu pake,
wale uliowakataza kuingia
kwenye kusanyiko lako.

11 [c]Watu wake wote wanalia kwa uchungu
watafutapo chakula;
wanabadilisha hazina zao kwa chakula
ili waweze kuendelea kuishi.
"Tazama, Ee BWANA, ufikiri,
kwa maana nimedharauliwa."

12 [d]"Je, si kitu kwenu, ninyi nyote mpitao kando?
Angalieni kote mwone.
Je, kuna maumivu kama maumivu yangu
yale yaliyotiwa juu yangu,
yale BWANA aliyoyaleta juu yangu
katika siku ya hasira yake kali?

13 [e]"Kutoka juu alipeleka moto,
akaushusha katika mifupa yangu.
Aliitandia wavu miguu yangu
na akanirudisha nyuma.
Akanifanya mkiwa,
na mdhaifu mchana kutwa.

14 [f]"Dhambi zangu zimefungwa kwenye nira,
kwa mikono yake zilifumwa pamoja.
Zimefika shingoni mwangu
na Bwana ameziondoa nguvu zangu.
Amenitia mikononi mwa wale
ambao siwezi kushindana nao.

15 [g]"Bwana amewakataa wapiganaji wa vita
wote walio kati yangu,
ameagiza jeshi dhidi yangu
kuwaponda vijana wangu wa kiume.
Katika shinikizo lake la divai Bwana amemkanyaga
Bikira Binti Yuda.

16 [h]"Hii ndiyo sababu ninalia
na macho yangu yanafurika machozi.
Hakuna yeyote aliye karibu kunifariji,
hakuna yeyote wa kuhuisha roho yangu.
Watoto wangu ni wakiwa
kwa sababu adui ameshinda."

17 [i]Sayuni ananyoosha mikono yake,
lakini hakuna yeyote wa kumfariji.
BWANA ametoa amri kwa ajili ya Yakobo
kwamba majirani zake wawe adui zake;
Yerusalemu umekuwa
kitu najisi miongoni mwao.

18 [j]"BWANA ni mwenye haki,
hata hivyo niliasi dhidi ya amri yake.
Sikilizeni, enyi mataifa yote,
tazameni maumivu yangu.

---

[a]**1:9** Isa 47:7; Eze 24:13; Yer 13:18; Mhu 4:1; Yer 16:7; Za 25:18; Kum 32:29
[b]**1:10** Neh 13:1; Kum 23:3; Yer 51:51; Isa 64:11; Za 74:7-8
[c]**1:11** Za 38:8; Yer 38:9; 37:21; 52:6
[d]**1:12** Yer 18:16; Isa 10:4; Yer 30:24; Dan 9:12; Isa 13:13; Mit 24:21; Lk 21:22
[e]**1:13** Ay 30:30; Za 102:3; Hab 3:16; Yer 44:6; Eze 12:13; Ay 18:8; Za 66:11; Hos 7:12
[f]**1:14** Isa 47:6; Yer 15:12; 32:5
[g]**1:15** Yer 37:10; Isa 41:2; 28:1; Yer 18:21; Ufu 14:19; Yer 14:17; Amu 6:11; Isa 63:3
[h]**1:16** Za 119:136; Ay 7:3; Yer 16:7; 13:17; 14:17; Isa 22:4; Mao 3:48-49
[i]**1:17** Yer 4:31; Kut 23:21; Law 18:25-28
[j]**1:18** 1Sam 12:14; Kum 28:32; Neh 9:33; Ezr 9:15; Kut 9:27; Dan 9:7

Wavulana wangu na wasichana wangu
wamekwenda uhamishoni.

19 [a]"Niliita washirika wangu
lakini walinisaliti.
Makuhani wangu na wazee wangu
waliangamia mjini
walipokuwa wakitafuta chakula
ili waweze kuishi.

20 [b]"Angalia, Ee BWANA, jinsi nilivyo katika dhiki!
Nina maumivu makali ndani yangu,
nami ninahangaika moyoni mwangu,
kwa kuwa nimekuwa mwasi sana.
Huko nje, upanga unaua watu,
ndani, kipo kifo tu.

21 [c]"Watu wamesikia ninavyolia kwa uchungu,
lakini hakuna yeyote wa kunifariji.
Adui zangu wote wamesikia juu ya dhiki yangu,
wanafurahia lile ulilolitenda.
Naomba uilete siku uliyoitangaza
ili wawe kama mimi.

22 [d]"Uovu wao wote na uje mbele zako;
uwashughulikie wao
kama vile ulivyonishughulikia mimi
kwa sababu ya dhambi zangu zote.
Kulia kwangu kwa uchungu ni kwingi
na moyo wangu umedhoofika."

2 [e] 1 [f]Tazama jinsi Bwana alivyomfunika Binti Sayuni
kwa wingu la hasira yake!
Ameitupa chini fahari ya Israeli
kutoka mbinguni mpaka duniani,
hakukumbuka kiti chake cha kuwekea miguu
katika siku ya hasira yake.

2 [g]Bila huruma Bwana ameyameza
makao yote ya Yakobo;
katika ghadhabu yake amebomoa
ngome za Binti Yuda.
Ameuangusha ufalme wake na wakuu wake
chini kwa aibu.

3 [h]Katika hasira kali amevunja
kila pembe[i] ya Israeli.
Ameuondoa mkono wake wa kuume
alipokaribia adui.
Amemteketeza Yakobo kama moto uwakao
ule uteketezao kila kitu kinachouzunguka.

4 [j]Ameupinda upinde wake kama adui,
mkono wake wa kuume uko tayari.
Kama vile adui amewachinja
wote waliokuwa wanapendeza jicho,
amemwaga ghadhabu yake kama moto
juu ya hema la Binti Sayuni.

5 [k]Bwana ni kama adui;
amemmeza Israeli.
Amemeza majumba yake yote ya kifalme
na kuangamiza ngome zake.
Ameongeza huzuni na maombolezo
kwa ajili ya Binti Yuda.

[a]**1:19** Mao 2:20; Yer 14:15; 22:20
[b]**1:20** Yer 4:19; Kum 32:25; Eze 7:15; Ay 20:2; Mao 2:11; Isa 16:11; Hos 11:8
[c]**1:21** Za 38:8; Mao 2:15; Yer 30:16; Isa 47:11; Za 6:6
[d]**1:22** Neh 4:5; Za 6:6
[e]Sura hii imetungwa kila beti likianzia, na pia kila mstari katika lile beti, na herufi ya alfabeti ya Kiebrania zikifuatana tangu Aleph (A) hadi Taw (T); zote ni 22.
[f]**2:1** Mao 3:44; Za 132:7; 1Nya 28:2; Yer 12:7; Za 99:5; Mt 11:23; 2Sam 1:19
[g]**2:2** Mao 3:43; Mik 5:11; Isa 25:12; Za 89:39-40; 21:9
[h]**2:3** Za 75:5; 74:11; Isa 42:25; Ay 16:15; Yer 21:4-5
[i]3 Pembe inawakilisha nguvu; pia 2:17.
[j]**2:4** Isa 63:10; Ay 3:23; Mao 3:12-13; Yer 7:20; Eze 24:16; 2Nya 34:21; Eze 20:34
[k]**2:5** Yer 30:14; Ay 13:24; Yer 9:17-20; Isa 29:2; Yer 7:20

6 [a]Ameharibu maskani yake kama
bustani,
ameharibu mahali pake pa
mkutano.
BWANA amemfanya Sayuni kusahau
sikukuu zake zilizoamriwa na
Sabato zake;
katika hasira yake kali amewadharau
mfalme na kuhani.

7 [b]Bwana amekataa madhabahu yake
na kuacha mahali patakatifu pake.
Amemkabidhi adui kuta
za majumba yake ya kifalme;
wamepiga kelele katika nyumba ya
BWANA
kama katika siku ya sikukuu
iliyoamriwa.

8 [c]BWANA alikusudia kuangusha
ukuta uliomzunguka Binti Sayuni.
Ameinyoosha kamba ya kupimia
na hakuuzuia mkono wake
usiangamize.
Alifanya maboma na kuta
ziomboleze,
vyote vikaharibika pamoja.

9 [d]Malango yake yamezama ardhini,
makomeo yake ameyavunja na
kuyaharibu.
Mfalme wake na wakuu wake
wamepelekwa uhamishoni
miongoni mwa mataifa,
sheria haipo tena,
na manabii wake hawapati tena
maono kutoka kwa BWANA.

10 [e]Wazee wa Binti Sayuni
wanaketi chini kimya,
wamenyunyiza mavumbi kwenye
vichwa vyao
na kuvaa nguo za gunia.
Wanawali wa Yerusalemu
wamesujudu hadi ardhini.

11 [f]Macho yangu yamedhoofika kwa
kulia,
nina maumivu makali ndani,
moyo wangu umemiminwa ardhini
kwa sababu watu wangu
wameangamizwa,
kwa sababu watoto na wanyonyao
wanazimia
kwenye barabara za mji.

12 Wanawaambia mama zao,
"Wapi mkate na divai?"
wazimiapo kama watu
waliojeruhiwa
katika barabara za mji,
maisha yao yadhoofikavyo
mikononi mwa mama zao.

13 [g]Ninaweza kusema nini kwa ajili
yako?
Nikulinganishe na nini,
ee Binti Yerusalemu?
Nitakufananisha na nini,
ili nipate kukufariji,
ee Bikira Binti Sayuni?
Jeraha lako lina kina kama bahari.
Ni nani awezaye kukuponya?

14 [h]Maono ya manabii wako
yalikuwa ya uongo na yasiyofaa
kitu,
hawakuifunua dhambi yako
ili kukuzuilia kwenda utumwani.
Maneno waliyokupa
yalikuwa ya uongo na ya
kupotosha.

15 [i]Wote wapitiao njia yako
wanakupigia makofi,

---

[a]**2:6** Yer 52:13; Sef 3:18; Yer 7:14; Isa 43:28; Mao 4:16; 5:12; Za 80:12; Isa 5:5; 1:8
[b]**2:7** Eze 7:1-2; Isa 64:10-11; Yer 7:12-14; Law 26:31; Yer 33:4-5; 52:13; Za 78:59-61; Mik 3:12; Yer 7:12-14; Mt 24:2
[c]**2:8** 2Fal 21:13; Isa 34:11; 3:26; Yer 39:8; Za 48:13; Amu 7:7
[d]**2:9** Yer 16:13; Amo 8:11-12; Hos 3:4; 2Nya 15:3; Yer 14:14; Isa 45:2; 2Fal 24:15; Kum 28:36; 2Fal 25:7; Za 74:9; Mik 3:6, 7
[e]**2:10** Ay 2:12-13; Isa 3:24, 26; Eze 27:30-31; Isa 15:3; Mao 3:28; 4:5; Isa 47:1-5
[f]**2:11** Isa 15:3; Ay 30:27; Za 22:14; Ay 16:13; Mao 3:48-51; Za 119:82; 6:7
[g]**2:13** Isa 37:22; Yer 14:17; 30:12-15; Dan 9:12; 2Fal 19:2; Ay 5:1
[h]**2:14** Isa 58:1; Yer 8:11; 20:6; Eze 13:3; Yer 28:3; 28:15; Eze 22:28
[i]**2:15** Hes 24:20; Eze 25:6; Nah 3:19; Za 45:11; Eze 16:14; Za 48:2; Yer 19:8; 1Fal 9:8

wanakudhihaki na kutikisa vichwa
vyao
kwa Binti Yerusalemu:
"Huu ndio ule mji ulioitwa
mkamilifu wa uzuri,
furaha ya dunia yote?"

16 [a]Adui zako wote wanapanua
vinywa vyao dhidi yako,
wanadhihaki na kusaga meno yao
na kusema, "Tumemmeza.
Hii ndiyo siku tuliyoingojea,
tumeishi na kuiona."

17 [b]BWANA amefanya lile alilolipanga;
ametimiza neno lake
aliloliamuru siku za kale.
Amekuangusha bila huruma,
amewaacha adui wakusimange,
ametukuza pembe ya adui yako.

18 [c]Mioyo ya watu
inamlilia Bwana.
Ee ukuta wa Binti Sayuni,
machozi yako na yatiririke kama
mto
usiku na mchana;
usijipe nafuu,
macho yako yasipumzike.

19 [d]Inuka, lia usiku,
zamu za usiku zianzapo;
mimina moyo wako kama maji
mbele za Bwana.
Mwinulie yeye mikono yako
kwa ajili ya maisha ya watoto
wako,
ambao wanazimia kwa njaa
kwenye kila mwanzo wa barabara.

20 [e]"Tazama, Ee BWANA, ufikirie:
Ni nani ambaye umepata
kumtendea namna hii?
Je, wanawake wakule wazao wao,
watoto waliowalea?
Je, kuhani na nabii auawe
mahali patakatifu pa Bwana?

21 [f]"Vijana na wazee hujilaza pamoja
katika mavumbi ya barabarani,
wavulana wangu na wasichana
wameanguka kwa upanga.
Umewaua katika siku ya hasira yako,
umewachinja bila huruma.

22 [g]"Kama ulivyoita siku ya karamu,
ndivyo ulivyoagiza hofu kuu
dhidi yangu kila upande.
Katika siku ya hasira ya BWANA
hakuna yeyote aliyekwepa au
kupona;
wale niliowatunza na kuwalea,
adui yangu amewaangamiza."

3 [h] 1 [i]Mimi ndiye mtu aliyeona mateso
kwa fimbo ya ghadhabu yake.
2 [j]Amenifukuzia mbali na kunifanya
nitembee
gizani wala si katika nuru;
3 [k]hakika, amegeuza mkono wake
dhidi yangu
tena na tena, mchana kutwa.

4 [l]Amefanya ngozi yangu na nyama
yangu kuchakaa
na ameivunja mifupa yangu.

---

[a]**2:16** Za 22:13; 56:2; Ay 16:19; Za 35:25; Eze 36:3; Mao 3:46
[b]**2:17** Kum 28:15-45; Eze 8:18; Isa 44:26; Mao 1:5; Law 26:16; Za 38:16
[c]**2:18** Za 119:145; Mao 1:16; 3:19; Yer 9:1; 14:7
[d]**2:19** Mk 13:35; 1Sam 1:15; Za 62:8; Isa 51:20; Neh 3:10; Isa 26:9; Mao 4:1
[e]**2:20** Kum 28:53; Eze 5:10; Mao 4:10; Yer 23:11-12; 19:9; Za 78:64; Yer 14:15; Kut 32:11; Law 26:29
[f]**2:21** Kum 32:25; 2Nya 36:17; Yer 13:14; Zek 11:6
[g]**2:22** Za 31:13; Yer 6:25; Ay 27:14; Hes 9:13; Yer 20:10
[h]Sura hii imetungwa kila beti likianzia, na pia kila mstari katika lile beti, na herufi ya alfabeti ya Kiebrania zikifuatana tangu Aleph (A) hadi Taw (T); zote ni 22.
[i]**3:1** Ay 19:21; Za 88:7; Yer 15:17-18
[j]**3:2** Ay 19:8; Za 82:5; Yer 4:23
[k]**3:3** Isa 5:25; Za 38:2
[l]**3:4** Za 51:8; Isa 38:13; Yer 50:17; Ay 30:30; Mao 4:8

5 [a]Amenizingira na kunizunguka
kwa uchungu na taabu.
6 [b]Amenifanya niishi gizani
kama wale waliokufa.

7 [c]Amenizungushia ukuta ili nisiweze
kutoroka,
amenifunga kwa minyororo
mizito.
8 [d]Hata ninapoita au kulia ili kuomba
msaada,
anakataa kupokea maombi yangu.
9 [e]Ameizuia njia yangu kwa mapande
ya mawe,
amepotosha njia zangu.

10 [f]Kama dubu aviziaye,
kama simba mafichoni,
11 ameniburuta kutoka njia,
akanirarua na kuniacha bila
msaada.
12 [g]Amevuta upinde wake
na kunifanya mimi niwe lengo
kwa ajili ya mishale yake.

13 Alinichoma moyo wangu kwa
mishale
iliyotoka kwenye podo lake.
14 [h]Nimekuwa kichekesho kwa watu
wangu wote,
wananidhihaki kwa wimbo
mchana kutwa.
15 [i]Amenijaza kwa majani machungu
na kunishibisha kwa nyongo.

16 [j]Amevunja meno yangu kwa
changarawe,
amenikanyagia mavumbini.
17 Amani yangu imeondolewa,
nimesahau kufanikiwa ni nini.
18 [k]Kwa hiyo nasema, "Fahari yangu
imeondoka
na yale yote niliyokuwa
nimetarajia kutoka kwa
BWANA."

19 Nayakumbuka mateso yangu na
kutangatanga kwangu,
uchungu na nyongo.
20 [l]Ninayakumbuka vyema,
nayo nafsi yangu imezimia ndani
yangu.
21 Hata hivyo najikumbusha neno hili
na kwa hiyo ninalo tumaini.

22 [m]Kwa sababu ya upendo mkuu wa
BWANA, hatuangamii,
kwa kuwa huruma zake hazikomi
kamwe.
23 [n]Ni mpya kila asubuhi,
uaminifu wako ni mkuu.
24 [o]Nimeiambia nafsi yangu, "BWANA
ni fungu langu,
kwa hiyo nitamngojea."

25 [p]BWANA ni mwema kwa wale ambao
tumaini lao ni kwake,
kwa yule ambaye humtafuta;
26 [q]ni vyema kungojea kwa utulivu
kwa ajili ya wokovu wa BWANA.
27 [r]Ni vyema mtu kuchukua nira
bado angali kijana.

28 [s]Na akae peke yake awe kimya,
kwa maana BWANA ameiweka juu
yake.
29 [t]Na azike uso wake mavumbini
bado panawezekana kuwa na
matumaini.

---

[a]**3:5** Yer 23:15
[b]**3:6** Isa 59:10; Za 143:3; 88:5-6
[c]**3:7** Ay 3:23; Yer 40:4
[d]**3:8** Kum 1:45; Ay 30:20; Za 22:2; 5:2
[e]**3:9** Ay 9:24; Hos 2:6; Isa 63:17
[f]**3:10** Ay 10:16; Hos 13:8; Amo 5:18-19
[g]**3:12** Mao 2:4; Ay 16:12; Za 38:2; 34:2
[h]**3:14** Mwa 38:23; Za 22:6-7; Ay 30:9; Neh 4:2-4; Mt 27:29-31; Yer 20:7
[i]**3:15** Yer 9:15
[j]**3:16** Mit 20:17
[k]**3:18** Ay 17:15; Za 31:22
[l]**3:20** Za 42:5; 43:5
[m]**3:22** Za 130:7; Mt 3:6; Neh 9:31; Ay 34:15; Za 130:1; Hos 11:9; Za 78:38; 57:10; Mal 3:6
[n]**3:23** Kut 34:6; Isa 33:2; Ebr 10:23
[o]**3:24** Za 16:5
[p]**3:25** Za 33:18; Isa 25:9; 30:18; Za 130:6
[q]**3:26** Za 37:7
[r]**3:27** Za 90:12
[s]**3:28** Yer 15:17
[t]**3:29** Yer 31:17; Ay 2:8; 42:6

30 [a]Na atoe shavu lake kwa yule
ampigaye,
na ajazwe na aibu.

31 [b]Kwa kuwa watu hawakatiliwi mbali
na Bwana milele.
32 [c]Ingawa huleta huzuni, ataonyesha
huruma,
kwa kuwa upendo wake usiokoma
ni mkuu.
33 [d]Kwa maana hapendi kuwaletea
mateso
au huzuni watoto wa wanadamu.

34 Kuwaponda chini ya nyayo
wafungwa wote katika nchi,
35 [e]Kumnyima mtu haki zake
mbele za Aliye Juu Sana,
36 [f]kumnyima mtu haki:
Je, Bwana asione mambo kama
haya?

37 [g]Nani awezaye kusema nalo
likatendeka
kama Bwana hajaamuru?
38 [h]Je, si ni kwenye kinywa cha Aliye
Juu Sana
ndiko yatokako maafa na mambo
mema?
39 [i]Mwanadamu yeyote aliye hai aweza
kulalamika
wakati anapoadhibiwa kwa ajili ya
dhambi zake?

40 [j]Tuzichunguze njia zetu na
kuzijaribu,
na tumrudie BWANA Mungu.

41 [k]Tuinue mioyo yetu pamoja na
mikono yetu
kwa Mungu mbinguni, na tuseme:
42 [l]"Tumetenda dhambi na kuasi
nawe hujasamehe.

43 [m]"Umejifunika mwenyewe kwa hasira
na kutufuatilia;
umetuchinja bila huruma.
44 [n]Unajifunika mwenyewe kwa wingu,
ili pasiwe na ombi
litakaloweza kupenya.
45 [o]Umetufanya takataka na uchafu
miongoni mwa mataifa.

46 [p]"Adui zetu wote wamefumbua
vinywa vyao
wazi dhidi yetu.
47 [q]Tumeteseka kwa hofu kuu na shida
ya ghafula,
uharibifu na maangamizi."
48 [r]Vijito vya machozi vinatiririka
kutoka machoni mwangu,
kwa sababu watu wangu
wameangamizwa.

49 Macho yangu yatatiririka machozi
bila kukoma,
bila kupata nafuu,
50 [s]hadi BWANA atazame chini
kutoka mbinguni na kuona.
51 Lile ninaloliona huniletea huzuni
nafsini
kwa sababu ya wanawake wote wa
mji wangu.

52 [t]Wale waliokuwa adui zangu bila
sababu
wameniwinda kama ndege.

[a]**3:30** Ay 16:10; Isa 50:6; Mik 5:1; Mt 5:39
[b]**3:31** Za 94:14; Isa 54:7
[c]**3:32** Za 106:43-45; Nah 1:12; Hos 11:8
[d]**3:33** Ay 37:23; Ebr 12:10; Yer 31:20; Eze 18:23
[e]**3:35** Mwa 14:18-22
[f]**3:36** Za 140:12; Mit 17:15; Hab 1:13; Yer 22:3
[g]**3:37** Mit 19:21; Za 33:9-11; Mit 21:30
[h]**3:38** Ay 2:10; Isa 45:7; Yer 32:42
[i]**3:39** Yer 30:15; Mik 7:9
[j]**3:40** 2Kor 13:5; Za 119:59; 139:23-24
[k]**3:41** Dan 9:5; Yer 14:20; 2Fal 24:4; Yer 5:7-9; Za 86:4
[l]**3:42** Dan 9:5
[m]**3:43** Mao 2:2, 17, 21; Za 35:6
[n]**3:44** Mao 2:1; Zek 7:13; Za 97:2; Isa 58:4
[o]**3:45** 1Kor 4:13
[p]**3:46** Za 22:13; Mao 2:16
[q]**3:47** Yer 48:43; Isa 24:17-18; 51:19
[r]**3:48** Yer 9:1; Mao 2:18
[s]**3:50** Za 14:2; 80:14; Isa 63:15
[t]**3:52** Za 35:7; 69:4

53 [a]Walijaribu kukomesha maisha
yangu ndani ya shimo
na kunitupia mawe;
54 [b]maji yalifunika juu ya kichwa
changu,
nami nikafikiri nilikuwa karibu
kukatiliwa mbali.

55 [c]Nililiitia jina lako, Ee BWANA,
kutoka vina vya shimo.
56 [d]Ulisikia ombi langu: "Usikizibie
masikio yako
kilio changu nikuombapo
msaada."
57 [e]Ulikuja karibu nilipokuita,
nawe ukasema, "Usiogope."

58 [f]Ee Bwana, ulichukua shauri langu,
ukaukomboa uhai wangu.
59 [g]Umeona, Ee BWANA, ubaya
niliotendewa.
Tetea shauri langu!
60 [h]Umeona kina cha kisasi chao,
mashauri yao yote mabaya dhidi
yangu.

61 Ee BWANA, umesikia matukano yao,
mashauri yao yote mabaya dhidi
yangu:
62 [i]kile adui zangu wanachonong'ona
na kunung'unikia
dhidi yangu mchana kutwa.
63 [j]Watazame! Wakiwa wameketi au
wamesimama,
wananidhihaki katika nyimbo zao.

64 [k]Uwalipe kile wanachostahili, Ee
BWANA,
kwa yale ambayo mikono yao
imetenda.
65 [l]Weka pazia juu ya mioyo yao,
laana yako na iwe juu yao!
66 Wafuatilie katika hasira na
uwaangamize
kutoka chini ya mbingu za
BWANA.

4 [m] 1 [n]Jinsi dhahabu ilivyopoteza
mng'ao wake,
dhahabu iliyo safi haing'ai!
Vito vya thamani vimetawanywa
kwenye mwanzo wa kila barabara.

2 [o]Wana wa Sayuni wenye thamani,
ambao mwanzo uzito wa thamani
yao
ulikuwa wa dhahabu,
sasa wanaangaliwa kama vyungu
vya udongo,
kazi ya mikono ya mfinyanzi!

3 [p]Hata mbweha hutoa matiti yao
kunyonyesha watoto wao,
lakini watu wangu wamekuwa wasio
na huruma
kama mbuni jangwani.

4 [q]Kwa sababu ya kiu ulimi wa mtoto
mchanga
umegandamana na kaakaa la
kinywa chake,
watoto huomba mkate,
lakini hakuna yeyote awapaye.

5 [r]Wale waliokula vyakula vya kifahari
ni maskini barabarani.

---

[a]**3:53** Yer 38:6; 37:16; Dan 6:17
[b]**3:54** Za 69:2; Yon 2:3-5; Eze 37:11; Za 88:5
[c]**3:55** Za 130:1; 2Nya 33:12; Yon 2:2; Za 18:5, 6
[d]**3:56** Rum 8:26; Za 116:1-2; 6:8
[e]**3:57** Isa 41:10; Yak 4:8; Za 46:1; 69:18; Isa 58:9
[f]**3:58** Yer 51:36; Za 34:22; Yer 50:34; 1Sam 25:39
[g]**3:59** Yer 18:19; Za 35:23
[h]**3:60** Yer 11:20; 18:18
[i]**3:62** Eze 36:3
[j]**3:63** Ay 30:9; Za 139:2
[k]**3:64** Za 28:4; Yer 51:6; 2Tim 4:14; Yer 11:20; Ufu 6:10
[l]**3:65** Kut 14:8; Kum 2:30; Isa 6:10; Za 8:3
[m]Sura hii imetungwa kila beti likianzia, na pia kila mstari katika lile beti, na herufi ya alfabeti ya Kiebrania zikifuatana tangu Aleph (A) hadi Taw (T); zote ni 22.
[n]**4:1** Eze 7:19
[o]**4:2** Isa 51:18; 2Kor 4:7
[p]**4:3** Ay 39:14-16
[q]**4:4** Mao 2:11-12; Za 22:15; 2Fal 18:31; Kum 28:48
[r]**4:5** Yer 6:2; Isa 3:26; Amo 6:3-7; Ay 24:8; Lk 15:16

Wale waliokuzwa wakivaa nguo za
zambarau
sasa wanalalia majivu.

6 [a]Adhabu ya watu wangu
ni kubwa kuliko ile ya Sodoma,
ambayo ilipinduliwa ghafula
bila kuwepo mkono wa msaada.

7 Wakuu wao walikuwa wameng'aa
kuliko theluji
na weupe kuliko maziwa,
miili yao ilikuwa myekundu kuliko
marijani,
kuonekana kwao kama yakuti
samawi.

8 [b]Lakini sasa ni weusi kuliko masizi;
hawatambulikani barabarani.
Ngozi yao imeshikamana juu ya
mifupa yao,
imekuwa mikavu kama fimbo.

9 [c]Wale waliouawa kwa upanga ni
bora
kuliko wale wanaokufa njaa;
wanateseka kwa njaa, wanatokomea
kwa kukosa chakula kutoka
shambani.

10 [d]Kwa mikono yao wenyewe
wanawake wenye huruma
wanapika watoto wao wenyewe,
waliokuwa chakula chao
watu wangu walipoangamizwa.

11 [e]BWANA ametoa nafasi kamilifu ya
ghadhabu yake;
ameimwaga hasira yake kali.
Amewasha moto katika Sayuni
ambao umeteketeza misingi yake.

12 [f]Wafalme wa dunia hawakuamini,
wala mtu yeyote wa duniani,
kwamba adui na watesi wangeweza
kuingia
kwenye malango ya Yerusalemu.

13 [g]Lakini hili lilitokea kwa sababu ya
dhambi za manabii wake,
na maovu ya makuhani wake,
waliomwaga ndani yake
damu ya wenye haki.

14 [h]Sasa wanapapasa papasa barabarani
kama watu ambao ni vipofu.
Wamenajisiwa kabisa kwa damu,
hata hakuna anayethubutu kugusa
mavazi yao.

15 [i]Watu wanawapigia kelele,
"Ondokeni! Ninyi ni najisi!
Ondokeni! Ondokeni! Msituguse!"
Wanapokimbia na kutangatanga
huku na huko,
watu miongoni mwa mataifa
wanasema,
"Hawawezi kukaa hapa zaidi."

16 [j]BWANA mwenyewe amewatawanya;
hawaangalii tena.
Makuhani hawaonyeshwi heshima,
wazee hawakubaliki.

17 [k]Zaidi ya hayo, macho yetu
yalichoka,
kwa kutazamia bure msaada;
tuliangalia kutoka minara yetu
kwa taifa lisiloweza kutuokoa.

18 [l]Watu walituvizia katika kila hatua
hata hatukuweza kutembea katika
barabara zetu.
Mwisho wetu ulikuwa karibu, siku
zetu zilikuwa zimetimia,
kwa maana mwisho wetu ulikuwa
umefika.

---

[a]**4:6** Mwa 19:25
[b]**4:8** Ay 30:28; Za 102:3-5; Mao 3:4
[c]**4:9** Yer 15:2; 16:4; 2Fal 25:3; Mao 5:10
[d]**4:10** Mao 2:20; Law 26:29; Kum 28:53-57; Eze 5:10; Yer 19:9
[e]**4:11** Yer 17:27; Kum 32:22; Yer 7:20; Ay 20:23; 2Nya 34:21; Eze 22:31
[f]**4:12** 1Fal 9:9; Yer 21:13; Kum 29:24
[g]**4:13** Yer 5:31; Eze 22:28; Mik 3:11; 2Fal 21:16; Mt 23:31
[h]**4:14** Isa 59:10; Yer 2:34; 19:4
[i]**4:15** Yer 44:14; Law 13:46; Mik 2:10
[j]**4:16** Isa 9:14-16; Mao 5:12
[k]**4:17** Mwa 15:18; Eze 29:16; Yer 37:7; Isa 20:5-6; 2Fal 24:7
[l]**4:18** Eze 7:2-12; Amo 8:2; Yer 51:33; 2Fal 25:4; Yer 51:33

19 [a]Waliotufuatia walikuwa wepesi
kuliko tai angani;
walitusaka juu milimani
na kutuvizia jangwani.

20 [b]Mpakwa mafuta wa BWANA, pumzi
ya uhai wetu hasa,
alinaswa katika mitego yao.
Tulifikiri kwamba chini ya kivuli
chake
tungeliweza kuishi miongoni mwa
mataifa.

21 [c]Shangilia na ufurahi, ee Binti
Edomu,
wewe unayeishi nchi ya Usi.
Lakini kwako pia kikombe
kitapitishwa,
Utalewa na kuvuliwa nguo ubaki
uchi.

22 [d]Ee Binti Sayuni, adhabu yako
itaisha,
hatarefusha muda wako wa kukaa
uhamishoni.
Lakini, ee Binti Edomu, ataadhibu
dhambi yako,
na atafunua uovu wako.

5 1 [e]Kumbuka, Ee BWANA,
yaliyotupata,
tazama, nawe uione aibu yetu.
2 [f]Urithi wetu umegeuziwa kwa
wageni,
na nyumba zetu kwa wageni.
3 [g]Tumekuwa yatima wasio na baba,
mama zetu wamekuwa kama
wajane.
4 [h]Ni lazima tununue maji
tunayokunywa,
kuni zetu zapatikana tu kwa
kununua.
5 [i]Wanaotufuatilia wapo kwenye
visigino vyetu,
tumechoka na hakuna pumziko.
6 [j]Tumejitolea kwa Misri na Ashuru
tupate chakula cha kutosha.
7 [k]Baba zetu walitenda dhambi na
hawapo tena,
na sisi tunachukua adhabu yao.
8 [l]Watumwa wanatutawala
na hakuna wa kutuokoa mikononi
yao.
9 Tunapata chakula chetu kwa
kuhatarisha maisha yetu
kwa sababu ya upanga jangwani.
10 [m]Ngozi yetu ina joto kama tanuru,
kwa sababu ya fadhaa itokanayo
na njaa.
11 [n]Wanawake wametendwa jeuri katika
Sayuni,
na mabikira katika miji ya Yuda.
12 Wakuu wametungikwa juu kwa
mikono yao,
wazee hawapewi heshima.
13 [o]Vijana wanataabika kwenye mawe
ya kusagia,
wavulana wanayumbayumba chini
ya mizigo ya kuni.
14 [p]Wazee wameondoka langoni la mji,
vijana wameacha kuimba nyimbo
zao.
15 [q]Furaha imeondoka mioyoni mwetu,
kucheza kwetu kumegeuka
maombolezo.

---

[a]**4:19** Kum 28:49; Law 26:36; Isa 5:26-28; Yer 52:7
[b]**4:20** 1Sam 26:9; 2Sam 19:21; Yer 39:5; Eze 19:4-8; 12:12-13; Mwa 2:7; Yer 52:9
[c]**4:21** Za 16:5; Yer 25:15; Eze 35:15; Hab 2:16; Mwa 10:23; Isa 34:6-10; Amu 1:11
[d]**4:22** Isa 40:2; Yer 33:8; Eze 25:12-14; Mal 1:4; Za 137:7
[e]**5:1** Za 44:13-16; 89:50
[f]**5:2** Za 79:1; Sef 1:13; Yer 17:4
[g]**5:3** Kut 22:24; Yer 15:8; 18:21
[h]**5:4** Isa 55:1; Eze 4:16-17; Isa 3:1
[i]**5:5** Isa 47:6; Neh 9:37; Yos 1:13
[j]**5:6** Yer 2:36; Mwa 24:2; Hos 5:13; 7:11; Yer 50:15; Hos 12:1
[k]**5:7** Yer 14:20; 16:12; Eze 8:2; Yer 31:29; Eze 18:2; Mt 23:32
[l]**5:8** Neh 5:15; Zek 11:6
[m]**5:10** Ay 30:30; Mao 4:8-9
[n]**5:11** Mwa 34:29; Zek 14:2; Isa 13:16
[o]**5:13** Amu 13:16; 16:21
[p]**5:14** Isa 24:8; Yer 7:34; 2Fal 25:18
[q]**5:15** Amu 8:10; Yer 25:10

16 [a]Taji imeanguka kutoka kichwani
petu.
Ole wetu, kwa maana tumetenda
dhambi!
17 [b]Kwa sababu hiyo, mioyo yetu
inazimia,
kwa sababu ya hayo, macho yetu
yamefifia,
18 [c]kwa ajili ya Mlima Sayuni, ambao
unakaa ukiwa,
nao mbweha wanatembea juu
yake.
19 [d]Wewe, Ee Bwana unatawala milele,
kiti chako cha enzi chadumu
kizazi hadi kizazi.
20 [e]Kwa nini watusahau siku zote?
Kwa nini umetuacha kwa muda
mrefu?
21 [f]Turudishe kwako mwenyewe, Ee
Bwana,
ili tupate kurudi.
Zifanye mpya siku zetu kama siku
za kale,
22 [g]isipokuwa uwe umetukataa kabisa
na umetukasirikia pasipo kipimo.

---

[a]**5:16** Yer 13:18; 14:20; Za 89:39; Ay 19:9; Isa 3:11
[b]**5:17** Ay 17:7; Za 6:7; 16:8; Yer 8:18
[c]**5:18** Isa 27:10; Mik 3:12; Za 74:2-4
[d]**5:19** 1Nya 16:31; Za 45:6; 102:22-27
[e]**5:20** Za 13:1; 44:24; 71:11
[f]**5:21** Isa 60:20-22; Za 80:3
[g]**5:22** Isa 64:9; Yer 6:30; Za 53:5; 60:12

# EZEKIELI

*Viumbe Hai Na Utukufu Wa* B*WANA*

1 [a]Katika mwaka wa thelathini, mwezi
wa nne, siku ya tano ya mwezi, wakati
nilipokuwa miongoni mwa hao waliokuwa
uhamishoni kando ya Mto Kebari, mbingu
zilifunguka nami nikaona maono ya Mungu.
2 [b]Katika siku ya tano ya mwezi, ilikuwa
mwaka wa tano wa kuhamishwa kwa
Mfalme Yehayakini, 3 [c]neno la BWANA
lilimjia Ezekieli kuhani, mwana wa
Buzi, kando ya Mto Kebari, katika nchi
ya Wakaldayo. Huko mkono wa BWANA
ulikuwa juu yake.
4 [d]Nilitazama, nikaona dhoruba kubwa
ikitoka kaskazini, wingu kubwa sana
pamoja likiwa na umeme wa radi likiwa
limezungukwa na mwanga mkali. Katikati
ya huo moto kulikuwa kama rangi ya
manjano ya chuma kinapokuwa ndani ya
moto. 5 [e]Katika ule moto kulikuwa na kitu
kinachofanana na viumbe vinne vyenye
uhai. Katika kuonekana kwake vilikuwa na
umbo mfano wa mwanadamu, 6 [f]lakini kila
kimoja kilikuwa na nyuso nne na mabawa
manne. 7 [g]Miguu yao ilikuwa imenyooka,
nyayo za miguu yao zilikuwa kama kwato za
miguu ya ndama, nazo zilimetameta kama
shaba iliyosuguliwa. 8 [h]Chini ya mabawa
yao katika pande zao nne walikuwa na
mikono ya mwanadamu. Wote wanne
walikuwa na nyuso na mabawa, 9 [i]nayo
mabawa yao yaligusana. Kila mmoja
alikwenda kuelekea mbele moja kwa moja,
hawakugeuka walipokuwa wanatembea.
10 [j]Kuonekana kwa nyuso zao kulikuwa
hivi: Kila mmoja wa wale wanne alikuwa
na uso wa mwanadamu na kwa upande
wa kulia kila mmoja alikuwa na uso wa
simba, upande wa kushoto alikuwa na uso
wa ng'ombe pia kila mmoja alikuwa na
uso wa tai. 11 [k]Hivyo ndivyo zilivyokuwa
nyuso zao. Mabawa yao yalikunjuliwa
kuelekea juu, kila mmoja alikuwa na
mabawa mawili ambayo kila moja liligusa
bawa la mwenzake kila upande na mabawa
mengine mawili yakifunika mwili wake.
12 [l]Kila mmoja alikwenda kuelekea mbele
moja kwa moja. Popote roho alipotaka
kwenda, ndipo walipokwenda pasipo
kugeuka. 13 [m]Kuonekana kwa vile viumbe
hai katikati kulikuwa kama makaa ya mawe
yanayowaka au kama mienge. Moto ule
ulikuwa ukienda mbele na nyuma katikati
ya vile viumbe, ulikuwa na mwangaza
mkali na katikati ya ule moto kulitoka
kimulimuli kama umeme wa radi. 14 [n]Vile
viumbe vilipiga mbio kwenda na kurudi,
kama vimulimuli vya umeme wa radi.
15 [o]Nilipokuwa nikitazama vile viumbe
hai, niliona gurudumu moja juu ya ardhi
kando ya kila kiumbe kikiwa na nyuso zake
nne. 16 [p]Hivi ndivyo ilivyokuwa kuonekana
kwa hayo magurudumu na muundo
wake: yaling'aa kama zabarajadi, nayo
yote manne yalifanana. Kila gurudumu
lilikuwa na gurudumu jingine ndani yake.
17 [q]Yalipokwenda yalielekea upande wowote
wa pande nne walipoelekea wale viumbe,
magurudumu hayakuzunguka wakati
viumbe vile vilipokwenda. 18 [r]Kingo zake
zilikuwa ndefu kwenda juu na za kutisha,
nazo zote nne zilijawa na macho pande
zote.

---

[a]**1:1** Kum 21:10; Mt 3:16; Eze 11:24-25; Mdo 7:56; Kut 24:10
[b]**1:2** 2Fal 24:15; 24:15; 24:12
[c]**1:3** 2Fal 3:15; Isa 8:11; 2Pet 1:21; Eze 24:24; 3:14, 22; 33:22
[d]**1:4** Yer 1:14; 23:19; Eze 8:2; Ay 38:1
[e]**1:5** Isa 6:2; Ufu 4:6; Dan 7:13
[f]**1:6** Eze 10:14
[g]**1:7** Dan 10:6; Ufu 1:15; Eze 40:3
[h]**1:8** Eze 10:8; 10:18, 21
[i]**1:9** Eze 10:22; 10:11; 1:11
[j]**1:10** Eze 10:4; Ufu 4:7; Hes 2:10
[k]**1:11** Isa 6:2
[l]**1:12** Eze 10:16-19; 10:22
[m]**1:13** Ufu 4:5; Mt 28:3; 2Sam 22:9
[n]**1:14** Zek 4:10; Za 29:7; Amu 13:20
[o]**1:15** Eze 3:13; 10:2; Dan 7:9
[p]**1:16** Dan 10:6; Kut 28:20
[q]**1:17** Eze 1:12; 1:19
[r]**1:18** Mit 15:3; Eze 10:12; Ufu 4:6

19 [a]Vile viumbe hai vilipokwenda,
magurudumu yaliyokuwa kando yao
yalisogea na wakati hivyo viumbe hai
vilipoinuka kutoka ardhini magurudumu
nayo yaliinuka. 20 [b]Mahali popote roho
alipokwenda wale viumbe nao walikwenda,
nayo magurudumu yaliinuka pamoja navyo,
kwa sababu roho ya vile viumbe hai alikuwa
ndani ya hayo magurudumu. 21 [c]Wakati
viumbe vile viliposogea, nayo magurudumu
yalisogea, viumbe viliposimama kimya,
nayo pia yalisimama kimya, viumbe
vilipoinuka juu ya nchi magurudumu
yaliinuliwa pamoja navyo kwa kuwa roho
ya hivyo viumbe hai alikuwa ndani ya hayo
magurudumu.

22 [d]Juu ya vichwa vya hao viumbe hai
palikuwa na kitu mfano wa eneo lililokuwa
wazi, lililokuwa angavu kabisa na lenye
kutisha. 23 Chini ya hiyo nafasi mabawa
yao yalitanda moja kuelekea jingine, kila
mmoja alikuwa na mabawa mengine mawili
yaliyofunika mwili wake. 24 [e]Viumbe wale
waliposogea nilisikia sauti ya mabawa yao,
kama ngurumo ya maji yaendayo kasi,
kama sauti ya Mwenyezi,[f] kama makelele
ya jeshi. Waliposimama kimya walishusha
mabawa yao.

25 Ndipo ikaja sauti toka juu ya ile
nafasi ya wazi iliyokuwa juu ya vichwa
vyao, waliposimama mabawa yao yakiwa
yameshushwa. 26 [g]Juu ya ile nafasi ya wazi
iliyokuwa juu ya vichwa vyao kulikuwa
na kitu mfano wa kiti cha enzi cha yakuti
samawi. Na juu ya kile kiti cha enzi
kulikuwa na umbo mfano wa mwanadamu.
27 [h]Nikaona kwamba kutokana na kile
nilichoona kama kiuno chake kuelekea
juu alionekana kama chuma inayowaka
kana kwamba imejaa moto na kuanzia
kiuno kwenda chini alionekana kama
moto na mwanga mkali ulimzunguka.
28 [i]Kama vile kuonekana kwa upinde wa
mvua mawinguni siku ya mvua, ndivyo
ulivyokuwa ule mng'ao uliomzunguka.

Hivi ndivyo ilivyokuwa kuonekana kwa utukufu wa BWANA. Nilipouona, nikaanguka kifudifudi, nikasikia sauti ya mtu anaongea.

*Wito Wa Ezekieli*

2 [j]Akaniambia, "Mwanadamu, simama
kwa miguu yako nami nitasema nawe."
2 [k]Alipokuwa akiongea nami, Roho akanijia
na kunisimamisha wima, nikamsikia
akisema nami.

3 [l]Akaniambia: "Mwanadamu,
ninakutuma kwa Waisraeli, kwa taifa asi
ambalo limeniasi mimi, wao na baba zao
wananikosea mimi hadi leo. 4 [m]Watu ambao
ninakutuma kwao ni wapotovu na wakaidi.
Waambie, 'Hivi ndivyo anavyosema
BWANA Mwenyezi.' 5 [n]Kama watasikiliza au
hawatasikiliza, kwa kuwa wao ni nyumba
ya kuasi, watajua nabii amekuwa miongoni
mwao. 6 [o]Nawe mwanadamu, usiwaogope
wao wala maneno yao, usiogope, ingawa
michongoma na miiba vinakuzunguka
na unaishi katikati ya nge. Usiogope
yale wasemayo wala usitishwe nao,
ingawa wao ni nyumba ya uasi. 7 [p]Wewe
lazima uwaambie maneno yangu, ikiwa
wanasikiliza au hawasikilizi, kwa kuwa wao
ni watu waasi. 8 [q]Lakini wewe mwanadamu,
sikiliza ninalokuambia. Usiwe mwenye

[a]**1:19** Eze 1:16, 17
[b]**1:20** Eze 1:12; 10:17
[c]**1:21** Eze 10:9, 12, 17
[d]**1:22** Eze 10:1, 5
[e]**1:24** 2Fal 7:6; Ufu 14:2; Dan 10:6; Za 18:13; 46:3; Eze 10:5; 43:2; Ufu 19:6
[f]24 Mwenyezi hapa ina maana ya Shaddai kwa Kiebrania.
[g]**1:26** Kut 24:10; Eze 10:1; Ufu 1:13; Isa 6:1; 1Fal 22:19; Yer 3:17
[h]**1:27** Eze 8:2
[i]**1:28** Mwa 9:13; Ufu 10:1; 4:2; 1:17; Hes 12:8; Kut 24:16; Dan 8:17; Hes 14:5; Lk 2:9; Kut 16:7
[j]**2:1** Dan 10:11; Mdo 26:16; Ay 25:6; Za 8:4; Eze 1:26; Mdo 9:6; 14:10
[k]**2:2** Eze 3:24; Dan 8:18; Amu 13:25
[l]**2:3** Yer 3:25; Eze 24:3; 20:8-24
[m]**2:4** Kut 32:9; Isa 9:9; Eze 3:7; Amo 7:15
[n]**2:5** Eze 3:11; 3:27; Yn 15:22; Eze 33:33; Yer 5:3
[o]**2:6** 1Pet 3:14; Yer 1:8, 17; Hes 33:55; Mik 7:4
[p]**2:7** Yer 7:27; 42:21; Eze 3:10-11; Mt 28:20
[q]**2:8** Isa 8:11; 50:5; Ufu 10:9; Za 81:10; Hes 20:10-13; Yer 15:16

kuasi kama hiyo nyumba ya kuasi. Fungua
kinywa chako na ule nikupacho.”
9 [a]Ndipo nikatazama, nami nikaona
mkono ulionyooshwa kunielekea. Nao
ulikuwa na ukurasa wa kitabu, 10 [b]ambao
aliukunjua mbele yangu. Pande zote
mbili ulikuwa umeandikwa maneno ya
maombolezo, vilio na ole.

3 [c]Naye akaniambia, “Mwanadamu, kula
kile kilichoko mbele yako, kula huu
ukurasa wa kitabu, kisha uende ukaseme
na nyumba ya Israeli.” 2 [d]Ndipo nikafungua
kinywa changu, naye akanilisha ule ukurasa
wa kitabu.
3 [e]Ndipo akaniambia, “Mwanadamu, kula
ukurasa huu wa kitabu ninaokupa ujaze
tumbo lako.” Kwa hiyo nikaula, ulikuwa
mtamu kama asali kinywani mwangu.
4 Kisha akaniambia, “Mwanadamu, sasa
nenda katika nyumba ya Israeli ukaseme
nao maneno yangu. 5 [f]Hukutumwa kwa taifa
lenye maneno ya kutatiza na lugha ngumu,
bali kwa nyumba ya Israeli. 6 [g]Sikukutuma
kwa mataifa mengi yenye maneno ya
kutatiza na lugha ngumu ambao maneno
yao hutayaelewa. Hakika ningekutuma
kwa watu hao, wangekusikiliza. 7 [h]Lakini
nyumba ya Israeli haitakusikiliza kwa kuwa
hawako radhi kunisikiliza mimi, kwa kuwa
nyumba yote ya Israeli ni wenye vipaji
vya nyuso vigumu na mioyo ya ukaidi.
8 [i]Tazama nimefanya uso wako mgumu
dhidi ya nyuso zao na kipaji cha uso wako
kigumu dhidi ya vipaji vya nyuso zao.
9 [j]Kama vile almasi ilivyo ngumu kuliko
gumegume, ndivyo nilivyokifanya kipaji
cha uso wako. Usiwaogope wala usiwahofu,
ijapokuwa ni nyumba ya kuasi.”
10 [k]Naye akaniambia, “Mwanadamu,
sikiliza kwa makini na uyatie moyoni
mwako maneno yote nitakayosema nawe.
11 [l]Kisha nenda kwa watu wa taifa lako
walio uhamishoni, ukaseme nao. Waambie,
‘Hivi ndivyo BWANA Mwenyezi asemavyo,’
kwamba watasikiliza au hawatasikiliza.”
12 [m]Ndipo Roho akaniinua, nikasikia sauti
kubwa nyuma yangu ya ngurumo. (Utukufu
wa BWANA na utukuzwe katika mahali
pa makao yake!) 13 [n]Ilikuwa ni sauti ya
mabawa ya wale viumbe hai yakisuguana
moja kwa jingine, sauti kama ya ngurumo.
14 [o]Ndipo Roho aliponiinua na kunipeleka
mbali. Nikaenda nikiwa na uchungu na
hasira moyoni mwangu, nao mkono wa
BWANA ukiwa juu yangu. 15 [p]Nikafika kwa
wale watu waliokuwa uhamishoni huko
Tel-Abibu karibu na Mto Kebari. Nikakaa
miongoni mwao kwa muda wa siku saba,
nikiwa nimejawa na mshangao.

### *Onyo Kwa Israeli*

16 [q]Mwishoni mwa hizo siku saba neno la
BWANA likanijia kusema: 17 [r]“Mwanadamu,
nimekufanya uwe mlinzi wa nyumba ya
Israeli, kwa hiyo sikia neno nisemalo,
ukawape onyo litokalo kwangu.
18 [s]Nimwambiapo mtu mwovu, ‘Hakika
utakufa,’ na wewe usipomwonya mtu huyo
au kumshauri aache njia zake mbaya ili
kuokoa maisha yake, huyo mtu mwovu
atakufa katika dhambi yake na damu
yake nitaidai mkononi mwako. 19 [t]Lakini
ukimwonya mtu mwovu naye akakataa
kuacha uovu wake na njia zake mbaya,
atakufa katika dhambi yake, lakini wewe
utakuwa umejiokoa nafsi yako.

---

[a]**2:9** Eze 8:3; Yer 1:9; Za 40:7; Yer 36:4; Ufu 5:1-5; 10:8-10
[b]**2:10** Isa 3:11; Ufu 8:13
[c]**3:1** Eze 2:8, 9
[d]**3:2** Hes 11:25; Amu 13:25; Neh 9:30
[e]**3:3** Yer 15:16; Za 19:10; Ufu 10:9-10; Za 19:10
[f]**3:5** Isa 28:11; Yn 1:2
[g]**3:6** Yn 3:5-10; Mt 11:21-23
[h]**3:7** Isa 48:4; Yn 15:20-23; Yer 7:27; Eze 2:4
[i]**3:8** Yer 1:18; 15:20
[j]**3:9** Isa 50:7; 48:4; Mik 3:8; Eze 2:6; 4:6; Yer 5:3
[k]**3:10** Ay 22:22
[l]**3:11** Eze 43:5; Mdo 8:39; Eze 8:3
[m]**3:12** Eze 3:14; 8:3; 43:5
[n]**3:13** Eze 1:24; 10:5, 16-17; 1:15
[o]**3:14** 1Fal 18:12; Isa 8:11; Eze 37:1
[p]**3:15** Mwa 50:10; Ay 2:13
[q]**3:16** Yer 42:7
[r]**3:17** Isa 52:8; Yer 6:17; Wim 5:7; Eze 11:4; Yer 1:17; Isa 58:1
[s]**3:18** Eze 33:6; Rum 1:16; Mwa 2:17; Yn 8:21
[t]**3:19** 2Fal 17:13; 1Tim 4:14-16; Za 7:12; Yer 42:16; Eze 14:14-20; Mdo 18:6

20 [a]“Tena, mtu mwenye haki akiacha haki
yake na kutenda maovu, nami nikaweka
kikwazo mbele yake mtu huyo atakufa.
Kwa kuwa hukumwonya, atakufa katika
dhambi yake. Mambo ya haki aliyotenda,
hayatakumbukwa, damu yake nitaidai
mkononi mwako. 21 [b]Lakini ukimwonya
mwenye haki asitende dhambi na akaacha
kutenda dhambi, hakika ataishi kwa sababu
alipokea maonyo na utakuwa umejiokoa
nafsi yako.”
22 [c]Mkono wa BWANA ulikuwa juu yangu
huko, naye akaniambia, “Simama uende
mpaka sehemu tambarare, nami nitasema
nawe huko.” 23 [d]Kwa hiyo niliinuka nikaenda
mpaka mahali pa tambarare. Utukufu wa
BWANA ulikuwa umesimama huko, kama
utukufu ule nilioouona kando ya Mto Kebari,
nami nikaanguka kifudifudi.
24 [e]Ndipo Roho akaja ndani yangu
akanisimamisha kwa miguu yangu.
Akasema nami akaniambia: “Nenda
ukajifungie ndani ya nyumba yako.
25 [f]Nawe, ee mwanadamu, watakufunga
kwa kamba, watakufunga ili usiweze kutoka
na kuwaendea watu. 26 [g]Nitaufanya ulimi
wako ushikamane kwenye kaa la kinywa
chako, ili uwe kimya usiweze kuwakemea,
wajapokuwa ni nyumba ya kuasi. 27 [h]Lakini
nitakaposema nawe, nitafungua kinywa
chako nawe utawaambia, ‘Hili ndilo BWANA
Mwenyezi asemalo.’ Yeyote atakayesikiliza
na asikilize, na yeyote atakayekataa na
akatae; kwa kuwa wao ni nyumba ya kuasi.

*Kuzingirwa Kwa Yerusalemu Kwaonyeshwa Kwa Mfano*

4 “Mwanadamu, sasa chukua tofali,
uliweke mbele yako na uchore juu yake
ramani ya mji wa Yerusalemu. 2 [i]Kisha
uuzingire: Simamisha askari dhidi yake
kuuzunguka, uzunguke kwa majeshi, weka
kambi dhidi yake pande zote pamoja na
magogo ya kubomolea boma vitani. 3 [j]Kisha
chukua bamba la chuma, ukalisimamishe
liwe kama ukuta wa chuma kati yako na
huo mji, nawe uuelekeze uso wako. Huo
mji utakuwa katika hali ya kuzingirwa,
nawe utauzingira. Hii itakuwa ishara kwa
nyumba ya Israeli.
4 “Kisha ulale kwa upande wako wa
kushoto na uweke dhambi za nyumba ya
Israeli juu yake. Utazibeba dhambi zao kwa
idadi ya siku utakazolala kwa huo upande
mmoja. 5 [k]Nimekupangia idadi ya siku kama
miaka ya dhambi yao. Kwa hiyo kwa siku
390 utabeba dhambi za nyumba ya Israeli.
6 [l]“Baada ya kumaliza hili, lala chini
tena, wakati huu ulale chini kwa upande
wa kuume, uchukue dhambi za nyumba ya
Yuda. Nimekupangia siku arobaini, siku
moja kwa kila mwaka mmoja. 7 [m]Geuza
uso wako uelekeze kwenye kuzingirwa
kwa Yerusalemu na mkono wako ambao
haukuvikwa nguo tabiri dhidi yake.
8 [n]Nitakufunga kwa kamba ili usiweze
kugeuka kutoka upande mmoja hadi upande
mwingine, mpaka hapo utakapokuwa
umetimiza siku za kuzingirwa kwako.
9 [o]“Chukua ngano na shayiri, maharagwe
na dengu, mtama na mawele, uviweke
na kuvihifadhi vyote kwenye gudulia la
kuhifadhia, na uvitumie kujitengenezea
mkate. Utaula mkate huo kwa hizo siku
390 utakazokuwa umelala kwa upande
mmoja. 10 [p]Pima shekeli ishirini[q] za chakula
utakachokula kwa kila siku, nawe utakula

[a]**3:20** 2Pet 2:20; Za 125:5; Eze 18:24; Yer 34:16; Isa 8:14; Law 26:37
[b]**3:21** Mdo 20:31; Rum 2:7
[c]**3:22** Eze 8:4; Mdo 9:6
[d]**3:23** Mwa 17:3; Eze 1:28
[e]**3:24** Eze 2:2; Yer 15:17
[f]**3:25** Eze 4:8
[g]**3:26** Eze 33:22; Hos 4:4; Eze 24:27; Za 22:15; Eze 2:5
[h]**3:27** Eze 24:27; 29:21; Ufu 22:11; Eze 12:3; 33:22
[i]**4:2** Yer 6:6; Dan 11:15; Eze 21:22; Yer 33:4; Eze 17:17
[j]**4:3** Eze 20:3; Yer 13:1-7; 39:1; Isa 8:18; Law 2:5; Eze 20:46; 12:3-6
[k]**4:5** Hes 14:34
[l]**4:6** Hes 14:34; Dan 12:11-12; 9:24-26; Kut 28:38
[m]**4:7** Eze 6:2; 13:17
[n]**4:8** Eze 3:25
[o]**4:9** Isa 28:25
[p]**4:10** Kut 30:13
[q]10 Shekeli 20 ni sawa na gramu 200.

kwa wakati uliopangwa. 11 [a]Pia pima maji
moja ya sita ya hini,[b] nawe utakunywa
kwa wakati uliopangwa. 12 [c]Nawe utakula
chakula kama vile ambavyo ungekula mkate
wa shayiri, uoke mkate mbele ya macho ya
watu, ukitumia kinyesi cha mwanadamu."
13 [d]BWANA akasema, "Hivi ndivyo watu wa
Israeli watakavyokula chakula kilicho najisi
miongoni mwa mataifa ninakowapeleka."

14 [e]Ndipo nikasema, "Sivyo BWANA
Mwenyezi! Kamwe mimi sijajitia unajisi.
Tangu ujana wangu hadi sasa sijala kamwe
kitu chochote kilichokufa au kilichoraruliwa
na wanyama wa mwituni. Hakuna nyama
yeyote najisi iliyoingia kinywani mwangu."

15 Akasema, "Vema sana, basi
nitakuruhusu uoke mkate wako kwa
kutumia kinyesi cha ng'ombe badala ya
kinyesi cha mwanadamu."

16 [f]Ndipo Mungu akaniambia,
"Mwanadamu, mimi nitakatilia mbali
upatikanaji wa chakula katika Yerusalemu.
Watu watakula chakula cha kupimwa kwa
wasiwasi pamoja na maji ya kupimiwa kwa
kukata tamaa, 17 [g]kwa kuwa chakula na
maji vitakuwa adimu. Watastajabiana kila
mmoja, nao watadhoofika kwa sababu ya
dhambi yao.

### *Upanga Dhidi Ya Yerusalemu*

5 [h]"Mwanadamu, sasa chukua upanga
mkali na uutumie kama wembe wa
kinyozi ili kunyolea nywele za kichwa
chako na ndevu zako. Kisha uchukue
mizani ya kupimia ukazigawanye nywele
hizo. 2 [i]Wakati siku zako za kuzingirwa
zitakapokwisha, choma theluthi moja ya
hizo nywele zako kwa moto ndani ya mji.
Chukua theluthi nyingine ya hizo nywele
uzipige kwa upanga kuuzunguka mji wote
na theluthi nyingine ya mwisho utaitawanya
kwa upepo. Kwa kuwa nitawafuatia kwa
upanga uliofutwa. 3 [j]Lakini chukua nywele
chache uzifungie ndani ya pindo la vazi
lako. 4 [k]Tena chukua nywele nyingine
chache uzitupe motoni uziteketeze. Moto
utaenea kutoka humo na kufika katika
nyumba yote ya Israeli.

5 [l]"Hili ndilo BWANA Mwenyezi asemalo:
Huu ndio Yerusalemu ambao nimeuweka
katikati ya mataifa ukiwa umezungukwa
na nchi pande zote. 6 [m]Lakini katika uovu
wake umeasi sheria na amri zangu kuliko
mataifa na nchi zinazouzunguka. Umeasi
sheria zangu wala haukufuata amri zangu.

7 [n]"Kwa hiyo hili ndilo BWANA Mwenyezi
asemalo: Ninyi mmekuwa wakaidi kuliko
mataifa yanayowazunguka na hamkufuata
amri zangu wala kuzishika sheria zangu.
Wala hamkuweza hata kuzifuata kawaida
za mataifa yanayowazunguka.

8 [o]"Kwa hiyo, hili ndilo BWANA
Mwenyezi asemalo, Mimi mwenyewe, niko
kinyume nanyi Yerusalemu, nitawapiga
kwa adhabu yangu mbele ya mataifa.
9 [p]Kwa ajili ya sanamu zenu zote za
machukizo, nitawafanyia kile ambacho
kamwe sijawafanyia kabla wala kamwe
sitawafanyia tena. 10 [q]Kwa hiyo katikati
yenu baba watakula watoto wao na
watoto watakula baba zao. Nitawapiga
kwa adhabu, nami nitawatawanya watu
wenu walionusurika pande zote za dunia.

[a]**4:11** Eze 4:16
[b]11 Moja ya sita ya hini ni sawa na mililita (ml) 600.
[c]**4:12** Isa 36:12
[d]**4:13** Hos 9:3; Amo 7:17
[e]**4:14** Eze 20:49; Law 11:39; Dan 1:8; Mdo 10:14; Kum 14:3; Hos 9:3-4; Eze 20:49
[f]**4:16** Za 105:16; Eze 5:16; Law 26:26; Isa 3:1; Eze 12:19
[g]**4:17** Law 26:39; Eze 33:10; 24:23; 5:16; 12:18-19; Amo 4:8
[h]**5:1** Law 21:5; Isa 7:20; Eze 44:20; Hes 6:5; 2Sam 10:14
[i]**5:2** Law 26:33; Yer 39:1-2; Zek 13:8; Yer 21:10; Eze 15:7; Yer 13:24; 9:16
[j]**5:3** Yer 40:6; 39:10; 2Fal 25:12; Za 74:11
[k]**5:4** Eze 10:7; 15:7
[l]**5:5** Kum 4:6; Mao 1:1; Eze 16:14
[m]**5:6** Neh 9:17; Zek 7:11; Rum 1:25; Eze 16:16; 2Fal 17:15; Yer 11:10
[n]**5:7** 2Fal 21:9; 2Nya 33:9; Yer 2:10-11
[o]**5:8** Yer 21:5; Zek 14:2; Yer 24:9; Eze 11:9; 15:7
[p]**5:9** Dan 9:12; Amo 3:2; Mt 24:21
[q]**5:10** Law 26:29; Mao 2:20; Yer 13:14; Zek 2:6; Za 44:11; Eze 12:14

11 [a]Kwa hiyo hakika kama niishivyo, asema
BWANA Mwenyezi, kwa kuwa mmenajisi
mahali pangu patakatifu kwa sanamu zenu
mbaya sana na desturi zenu za machukizo,
mimi mwenyewe nitaondoa fadhili zangu
kwenu. 12 [b]Theluthi ya watu wako watakufa
kwa tauni au kwa njaa humu ndani yako,
theluthi nyingine itaanguka kwa upanga
nje ya kuta zako, nayo theluthi nyingine
nitaitawanya kwenye pande nne kuwafuatia
kwa upanga uliofutwa.
13 [c]“Ndipo hasira yangu itakapokoma
na ghadhabu yangu dhidi yao itatulia,
nami nitakuwa nimelipiza kisasi. Baada
ya kuimaliza ghadhabu yangu juu yao,
watajua kuwa mimi BWANA nimenena
katika wivu wangu.
14 [d]“Nitakuangamiza na kukufanya kitu
cha kudharauliwa miongoni mwa mataifa
yanayokuzunguka, machoni pa watu wote
wapitao karibu nawe. 15 [e]Utakuwa kitu cha
kudharauliwa na cha aibu, cha dhihaka,
ovyo na kitu cha kutisha kwa mataifa
yanayokuzunguka, nitakapokupiga kwa
adhabu yangu katika hasira na ghadhabu
yangu kwa kukukemea kwa ukali. Mimi
BWANA nimesema. 16 [f]Nitakapokupiga kwa
mishale yangu ya kufisha na yenye kuharibu
ya njaa, nitaipiga ili kukuangamiza.
Nitaleta njaa zaidi na zaidi juu yako na
kukomesha upatikanaji wa chakula kwako.
17 [g]Nitapeleka njaa na wanyama wa mwituni
dhidi yenu, navyo vitawaacha bila watoto.
Tauni na umwagaji wa damu utapita
katikati yenu, nami nitaleta upanga juu
yenu. Mimi BWANA nimenena haya.”

### *Unabii Dhidi Ya Milima Ya Israeli*

6 Neno la BWANA likanijia kusema,
2 [h]“Mwanadamu, elekeza uso wako
kukabili milima ya Israeli, utabiri dhidi yake
3 na useme: ‘Ee milima ya Israeli, sikia neno
la BWANA Mwenyezi. Hili ndilo BWANA
Mwenyezi aliambiayo milima na vilima,
magenge na mabonde: Ninakaribia kuleta
upanga dhidi yenu, nami nitapaharibu
mahali penu pote pa juu pa kuabudia
miungu. 4 [i]Madhabahu yenu yatabomolewa
na madhabahu yenu ya kufukizia uvumba
yatavunjavunjwa, nami nitawachinja watu
wenu mbele ya sanamu zenu. 5 [j]Nitazilaza
maiti za Waisraeli mbele ya sanamu zao,
nami nitatawanya mifupa yenu kuzunguka
madhabahu yenu. 6 [k]Popote mnapoishi,
miji hiyo itafanywa ukiwa na mahali pa
juu pa kuabudia miungu patabomolewa,
ili madhabahu yenu ifanywe ukiwa na
kuharibiwa, sanamu zenu zitavunjavunjwa
na kuharibiwa, madhabahu yenu ya
kufukizia uvumba yatabomolewa na kila
mlichokifanya kitakatiliwa mbali. 7 [l]Watu
wenu watachinjwa katikati yenu, nanyi
mtatambua Mimi ndimi BWANA.
8 [m]“ ‘Lakini nitawabakiza hai baadhi yenu,
kwa kuwa baadhi yenu watanusurika kuuawa
watakapokuwa wametawanyika katika nchi
na mataifa. 9 [n]Ndipo katika mataifa ambamo
watakuwa wamechukuliwa mateka, wale
ambao watanusurika watanikumbuka, jinsi
ambavyo nimehuzunishwa na mioyo yao ya
uzinzi, ambayo imegeukia mbali nami na
macho yao ambayo yametamani sanamu
zao. Watajichukia wenyewe kwa ajili ya
uovu walioutenda na kwa ajili ya desturi
zao za kuchukiza. 10 [o]Nao watajua kuwa

---

[a]**5:11** Eze 7:20; 8:6; 2Nya 36:14; Eze 11:18-21; Yer 16:18; Ay 27:22; Hes 14:21; Law 15:2; 15:31; Mao 2:17
[b]**5:12** Ufu 6:8; Za 107:39; Eze 12:14; Zek 13:8; Eze 6:11-12; Yer 21:9; 13:24
[c]**5:13** 2Nya 12:7; Ay 20:23; Isa 1:24; Mao 4:11; Eze 21:17; 24:13; Hos 10:10
[d]**5:14** Mik 3:12; Isa 64:11; Neh 2:17; Za 74:3-10; Eze 22:4; Dan 9:16
[e]**5:15** Kum 28:20; 1Fal 9:7; Yer 23:40; Eze 25:17; Mao 2:15; Isa 43:28; Yer 22:8-9
[f]**5:16** Law 26:26; Kum 32:24; Eze 14:21
[g]**5:17** Eze 38:23; Law 26:25; Eze 28:22
[h]**6:2** Eze 36:1; Mik 6:1; Eze 18:6; 4:7; 36:4; Law 26:30
[i]**6:4** 2Nya 14:5; Yer 44:28; Eze 9:4; 14:3
[j]**6:5** Hes 19:16; Za 53:5; Yer 8:1-2
[k]**6:6** Mik 1:7; Zek 13:2; Law 26:30; Isa 6:11; 1Sam 5:4; Kut 12:20; Hos 10:8; Eze 30:13
[l]**6:7** Eze 9:7; 6:13; 7:4, 9; 11:10, 12; 12:15
[m]**6:8** Za 68:20; 44:11; Yer 44:28; Mwa 11:4; Isa 6:13; Eze 7:16; 12:16; 14:22
[n]**6:9** Za 78:40; Yer 8:21; Isa 7:13; Mik 5:13; Kut 22:20; Ay 42:6; Eze 36:31
[o]**6:10** Zek 10:9; Eze 20:43; Kum 28:52; Yer 40:2

Mimi ndimi Bwana, sikuwaonya bure kuwa
nitaleta maafa hayo yote juu yao.
11 [a]“ ‘Hili ndilo Bwana Mwenyezi asemalo:
Piga makofi, kanyaga chini kwa mguu na
upige kelele, “Ole!” kwa sababu ya maovu
yote na machukizo yote yanayofanywa na
nyumba ya Israeli, kwa kuwa wataanguka
kwa upanga, njaa na tauni. 12 [b]Yeye aliye
mbali sana atakufa kwa tauni, naye
aliye karibu atauawa kwa upanga, naye
yule atakayenusurika na kubaki atakufa
kwa njaa. Hivyo ndivyo nitakavyotimiza
ghadhabu yangu dhidi yao. 13 [c]Nao watajua
kwamba Mimi ndimi Bwana, wakati maiti
za watu wao zitakapokuwa zimelala katikati
ya sanamu zao kuzunguka madhabahu yao,
juu ya kila kilima kilichoinuka na juu ya
vilele vyote vya milima, chini ya kila mti
uliotanda na kila mwaloni wenye majani,
yaani, sehemu walizofukizia uvumba kwa
sanamu zao zote. 14 [d]Nami nitanyoosha
mkono wangu dhidi yao na kuifanya nchi
yao ukiwa, kuanzia jangwani hadi Dibla,
kila mahali wanapoishi. Ndipo watakapojua
ya kwamba Mimi ndimi Bwana.’ ”

*Mwisho Umewadia*

7 Neno la Bwana likanijia kusema:
2 [e]“Mwanadamu, hili ndilo Bwana
Mwenyezi asemalo kwa nchi ya Israeli:
Mwisho! Mwisho umekuja juu ya pembe nne
za nchi. 3 [f]Sasa mwisho umekuja juu yenu
nami nitamwaga hasira yangu dhidi yenu.
Nitawahukumu sawasawa na matendo yenu
na kuwalipiza kwa ajili ya desturi zenu zote
za kuchukiza. 4 [g]Sitawaonea huruma wala
sitawarehemu, hakika nitalipiza kwa ajili ya
matendo yenu na desturi zenu za machukizo
miongoni mwenu. Ndipo mtakapojua kuwa
Mimi ndimi Bwana.

5 [h]“Hili ndilo Bwana Mwenyezi asemalo:
Maafa! Maafa ambayo hayajasikiwa
yanakuja. 6 [i]Mwisho umewadia! Mwisho
umewadia! Umejiinua wenyewe dhidi yenu.
Umewadia! 7 [j]Maangamizi yamekuja juu
yenu, ninyi mnaoishi katika nchi. Wakati
umewadia, siku imekaribia, kuna hofu kuu
ya ghafula, wala si furaha, juu ya milima.
8 [k]Ninakaribia kumwaga ghadhabu yangu
juu yenu na kumaliza hasira yangu dhidi
yenu, nitawahukumu sawasawa na matendo
yenu na kuwalipiza kwa ajili ya desturi
zenu zote za machukizo. 9 [l]Sitawaonea
huruma wala sitawarehemu; nitawalipiza
sawasawa na matendo yenu na desturi zenu
za machukizo miongoni mwenu. Ndipo
mtajua kuwa Mimi ndimi Bwana ambaye
huwapiga kwa mapigo.

10 [m]“Siku imefika! Imewadia! Maangamizi
yamezuka ghafula, fimbo imechanua
majivuno yamechipua! 11 [n]Jeuri imeinuka
kuwa fimbo ya kuadhibu uovu, hakuna hata
mmoja wa hao watu atakayeachwa, hata
mmoja wa kundi lile, hakuna utajiri, hakuna
chenye thamani. 12 [o]Wakati umewadia, siku
imefika. Mnunuzi na asifurahi wala muuzaji
asihuzunike, kwa maana ghadhabu iko juu
ya kundi lote. 13 [p]Muuzaji hatajipatia tena
ardhi aliyoiuza wakati wote wawili wangali
hai, kwa kuwa maono kuhusu kundi lote
hayatatanguka. Kwa sababu ya dhambi
zao, hakuna hata mmoja atakayeokoa
maisha yake. 14 [q]Wajapopiga tarumbeta
na kuweka kila kitu tayari, hakuna hata
mmoja atakayekwenda vitani, kwa maana
ghadhabu yangu iko juu ya kundi lote.

---

[a]**6:11** Yer 42:22; Eze 22:13; 21:14-17; 25:6
[b]**6:12** Eze 5:12; 7:15; Ay 20:23
[c]**6:13** Isa 1:29; 57:5; Hos 4:13; Eze 18:6; Law 26:30; 1Fal 14:23; Yer 2:20; Eze 20:28
[d]**6:14** Kut 7:5; Ay 30:21; Eze 14:13; Isa 5:25; Yer 6:12; Eze 12:19; 20:34
[e]**7:2** Amo 8:2-10; Ufu 20:8; Mao 4:18
[f]**7:3** Eze 18:30; Mwa 6:13
[g]**7:4** Yer 13:14; Eze 5:11; 23:49
[h]**7:5** 2Fal 21:12
[i]**7:6** Eze 39:8
[j]**7:7** Sef 1:14; Mal 3:2; 1Pet 4:17; Ay 18:20; Isa 2:12; Amo 5:18-20; Eze 12:23
[k]**7:8** Hos 5:10; Nah 1:6; Eze 36:19; 14:19; 20:8, 21; 9:8; Isa 42:25
[l]**7:9** Yer 21:9; Isa 9:13; Eze 5:11; 22:31; Za 39:10
[m]**7:10** Za 89:32; Isa 10:5
[n]**7:11** Yer 16:6; Sef 1:18; Isa 58:4; Za 55:9
[o]**7:12** Isa 5:13-14; Eze 30:3; Isa 24:2
[p]**7:13** Law 25:24-25
[q]**7:14** Ay 39:24; Yer 25:38

[15] [a]“Nje ni upanga, ndani ni tauni na
njaa, wale walioko shambani watakufa
kwa upanga, nao wale waliomo mjini
njaa na tauni vitawala. [16] [b]Wale wote
watakaopona na kutoroka watakuwa
milimani, wakiomboleza kama hua wa
mabondeni, kila mmoja kwa sababu ya
dhambi zake. [17] [c]Kila mkono utalegea na kila
goti litakuwa dhaifu kama maji. [18] [d]Watavaa
nguo ya gunia na kufunikwa na hofu.
Nyuso zao zitafunikwa na aibu na nywele
za vichwa vyao zitanyolewa. [19] [e]Watatupa
fedha yao barabarani, nayo dhahabu yao
itakuwa najisi. Fedha yao na dhahabu yao
havitaweza kuwaokoa katika siku hiyo ya
ghadhabu ya Bwana. Hawatashibisha njaa
yao au kujaza matumbo yao kwa hiyo fedha
wala dhahabu, kwa sababu imewaponza
wajikwae dhambini. [20] [f]Walijivunia vito
vyao vizuri na kuvitumia kufanya sanamu
za machukizo na vinyago vya upotovu.
Kwa hiyo nitavifanya vitu hivyo kuwa
najisi kwao. [21] [g]Nitavitia vyote mikononi
mwa wageni kuwa nyara na kuwa vitu
vilivyotekwa mikononi mwa watu waovu
wa dunia, nao watavinajisi. [22] [h]Nitageuza
uso wangu mbali nao, nao waovu wa dunia
watapanajisi mahali pangu pa thamani,
wanyang’anyi watapaingia na kupanajisi.
[23] [i]“Andaa minyororo, kwa sababu
nchi imejaa umwagaji wa damu na mji
umejaa udhalimu. [24] [j]Nitaleta taifa ovu
kuliko yote ili kumiliki nyumba zao,
nitakomesha kiburi cha wenye nguvu na
mahali pao patakatifu patatiwa unajisi.
[25] [k]Hofu ya ghafula itakapokuja, watatafuta
amani, lakini haitakuwepo. [26] [l]Maafa juu
ya maafa yatakuja, tetesi ya mabaya juu
ya tetesi ya mabaya. Watajitahidi kupata
maono kutoka kwa nabii, mafundisho ya
sheria toka kwa kuhani yatapotea, vivyo
hivyo shauri kutoka kwa wazee. [27] Mfalme
ataomboleza, mwana wa mfalme atavikwa
kukata tamaa, nayo mikono ya watu wa
nchi itatetemeka. Nitawashughulikia
sawasawa na matendo yao na kwa kanuni
zao wenyewe nitawahukumu. Ndipo
watajua kwamba Mimi ndimi Bwana.”

### *Ibada Ya Sanamu Hekaluni*

8 [m]Katika siku ya tano ya mwezi wa sita
mwaka wa sita, baada ya kupelekwa
uhamishoni nilipokuwa nimeketi katika
nyumba yangu na wazee wa Yuda walikuwa
wameketi mbele yangu, mkono wa Bwana
Mwenyezi ulikuja juu yangu. [2] [n]Nikatazama,
nikaona umbo mfano wa mwanadamu.
Kutokana na kile kilichoonekana kuwa
kiuno chake kuelekea chini alifanana na
moto. Kuanzia kwenye kiuno kuelekea
juu sura yake kama chuma king’aavyo
kikiwa ndani ya moto. [3] [o]Akanyoosha kitu
kilichoonekana kama mkono, akaniinua
kwa kushika nywele za kichwa changu.
Roho akaniinua juu kati ya nchi na
mbingu nikiwa katika maono ya Mungu
akanichukua mpaka Yerusalemu, kwenye
ingilio la lango la upande wa kaskazini ya
ukumbi wa ndani, mahali iliposimama ile
sanamu ichocheayo wivu. [4] [p]Hapo mbele
yangu palikuwa na utukufu wa Mungu wa
Israeli, kama utukufu ule niliouona katika
maono kule ua wa ndani.
[5] [q]Kisha akaniambia, “Mwanadamu,

---

[a]**7:15** Kum 32:25; Yer 14:18; Mao 1:20; Eze 5:12; 33:27
[b]**7:16** Mwa 8:8; Isa 59:11; 10:20; Ezr 9:15; Yer 9:19; 41:16; 42:17
[c]**7:17** 2Fal 19:26; Isa 13:7; Dan 6:5; Yer 43:7; Eze 21:7; 22:14
[d]**7:18** Isa 15:2-3; Amo 8:10; Za 55:5; Yer 6:26; 4:8; 49:3; 48:37
[e]**7:19** Isa 42:25; Sef 1:18; Hos 4:5; Eze 3:20; Mit 11:4; Yoe 1:15; Eze 13:5; 14:3
[f]**7:20** Eze 5:11; 16:17; Yer 7:30; 10:3; Isa 2:20
[g]**7:21** 2Fal 24:13; Hes 14:3
[h]**7:22** Yer 2:27; 19:13; Eze 39:23-24; Za 74:7-8
[i]**7:23** 2Fal 21:16; Isa 1:15; Za 10:8; Eze 11:6; 22:9; Mwa 6:11
[j]**7:24** Mao 2:7; Eze 24:21; 28:7; 2Nya 7:20
[k]**7:25** Yer 6:14; 8:11; Eze 13:10-16
[l]**7:26** Kum 29:21; 31:17; Yer 4:20; 18:18; Amo 8:11; Mik 3:6; Mal 2:7-9; Isa 47:11; 3:11; Eze 18:20; Za 109:19
[m]**8:1** 2Fal 6:32; Eze 14:1; 33:31; 40:1; 24:1
[n]**8:2** Eze 1:4, 26-27; Dan 7:9
[o]**8:3** Eze 3:12; 11:1; Kut 20:5; Kum 32:16; Yer 7:30; Kut 24:10; Eze 2:9
[p]**8:4** Kut 24:16; Eze 1:28; 3:22
[q]**8:5** Za 78:58-60; Yer 4:1; 32:34

tazama kuelekea kaskazini.” Hivyo
nikatazama na kwenye ingilio upande wa
kaskazini wa lango la madhabahu, nikaona
sanamu hii ya wivu.
6 [a]Ndipo akaniambia, “Mwanadamu, je,
unaona yale wanayofanya, haya mambo
ya machukizo kabisa nyumba ya Israeli
wanayotenda hapa, ambayo yatanifanya
niende mbali na mahali pangu patakatifu?
Lakini utaona vitu ambavyo vinachukiza
zaidi hata kuliko hivi.”
7 Kisha akanileta mpaka ingilio la
ukumbi. Nikatazama, nami nikaona tundu
ukutani. 8 Akaniambia, “Mwanadamu, sasa
toboa kwenye ukuta huu.” Ndipo nikatoboa
ule ukuta, nikaona hapo pana mlango.
9 Naye akaniambia, “Ingia ndani, ukaone
maovu na machukizo wanayofanya humu.”
10 [b]Hivyo nikaingia ndani na kutazama,
nikaona kuta zote zimechorwa kila aina
ya vitu vitambaavyo na ya wanyama
wachukizao wa kila aina na sanamu
zote za nyumba ya Israeli. 11 [c]Mbele yao
walisimama wazee sabini wa nyumba ya
Israeli, naye Yaazania mwana wa Shafani
alikuwa amesimama miongoni mwao. Kila
mmoja alikuwa na chetezo mkononi na
moshi wa harufu nzuri ya uvumba ulikuwa
unapanda juu.
12 [d]Akaniambia, “Mwanadamu, umeona
wanayoyafanya wazee wa nyumba ya Israeli
gizani, kila mmoja kwenye sehemu yake
mwenyewe ya kufanyia ibada za sanamu
yake? Wao husema, ‘BWANA hatuoni,
BWANA ameiacha nchi.’ ” 13 Akasema tena,
“Bado utaona machukizo wanayofanya
ambayo ni makubwa kuliko haya.”
14 [e]Ndipo akanileta mpaka ingilio la
lango la kaskazini la nyumba ya BWANA,
nami nikaona wanawake wameketi hapo,
wakimwombolezea Tamuzi. 15 Akaniambia,
“Unaliona hili, mwanadamu? Utaona vitu
ambavyo ni machukizo kuliko hili.”
16 [f]Ndipo akanileta mpaka kwenye
ukumbi wa ndani wa nyumba ya BWANA,
nako huko katika ingilio la Hekalu, kati
ya baraza na madhabahu, walikuwepo
wanaume wapatao ishirini na watano.
Wakiwa wamelipa kisogo Hekalu la
BWANA na kuelekeza nyuso zao upande
wa mashariki, wakilisujudia jua huko
mashariki.
17 [g]Akaniambia, “Je, umeona hili
mwanadamu? Je, ni jambo dogo sana
kwa nyumba ya Yuda kufanya machukizo
wanayoyafanya hapa? Je, ni lazima pia
waijaze nchi dhuluma na kuendelea siku zote
kunikasirisha? Watazame wanavyonibania
pua kana kwamba ninanuka! 18 [h]Kwa
hiyo nitashughulika nao kwa hasira,
sitawaonea huruma wala kuwaachilia.
Wajapopiga makelele masikioni mwangu,
sitawasikiliza.”

*Waabudu Sanamu Wauawa*

9 Kisha nikamsikia akiita kwa sauti
kubwa akisema, “Walete wasimamizi
wa mji hapa, kila mmoja akiwa na silaha
mkononi mwake.” 2 [i]Nami nikaona watu
sita wakija toka upande wa lango la juu,
linalotazama kaskazini kila mmoja na silaha
za kuangamiza mkononi mwake. Pamoja
nao alikuwepo mtu aliyekuwa amevaa
mavazi ya kitani safi, naye alikuwa na
vifaa vya mwandishi akiwa amevishikilia
upande mmoja. Wakaingia ndani ya Hekalu
wakasimama pembeni mwa madhabahu
ya shaba.
3 [j]Basi utukufu wa Mungu wa Israeli
ukaondoka hapo juu ya makerubi, ulikokuwa
umekaa, ukaenda kwenye kizingiti cha

[a]**8:6** Eze 5:11; Kum 31:16; Hos 5:6
[b]**8:10** Kum 4:15-18; Yer 16:18; Amu 17:4-5; Eze 23:14; Yer 44:4; Kut 20:4
[c]**8:11** Hes 16:17; Yer 26:24; Law 10:1; Hes 16:17-35; Kut 3:16; Eze 11:1-2
[d]**8:12** 2Fal 21:16; Za 10:11; Ay 22:13; Isa 29:15; Eze 9:9
[e]**8:14** Eze 11:12
[f]**8:16** Yoe 2:17; Kum 4:19; Ay 31:28; Mwa 1:16; Yer 2:27; Eze 40:6; 9:6
[g]**8:17** Mwa 6:11; Ezr 9:6; Hes 11:33; 1Fal 14:9; Eze 16:2; 16:26
[h]**8:18** Yer 13:14; 44:6; Eze 24:14; Isa 1:15; Mik 3:4; Mit 1:28; 1Sam 8:18; Isa 58:4; Eze 9:10
[i]**9:2** Dan 10:5; 12:6; Ufu 15:6; Eze 10:2; Law 16:4
[j]**9:3** 1Sam 4:21; Eze 10:4; 11:22

Hekalu. Ndipo BWANA akamwita yule
mtu aliyevaa kitani safi aliyekuwa na
vifaa vya mwandishi akiwa amevishikilia
upande wake mmoja, 4 [a]akamwambia, "Pita
katika mji wote wa Yerusalemu ukaweke
alama juu ya vipaji vya nyuso za wale watu
wanaohuzunika na kuomboleza kwa sababu
ya machukizo yote yanayotendeka katika
mji huu."
5 [b]Nikiwa ninasikia, akawaambia wale
wengine, "Mfuateni anapopita katika
mji wote mkiua, pasipo huruma wala
masikitiko. 6 [c]Waueni wazee, vijana wa
kiume na wa kike, wanawake na watoto,
lakini msimguse mtu yeyote mwenye
alama. Anzieni katika mahali pangu
patakatifu." Kwa hiyo wakaanza na wale
wazee waliokuwa mbele ya Hekalu.
7 [d]Ndipo akawaambia, "Linajisini Hekalu
na mkazijaze kumbi zake maiti za wale
waliouawa. Nendeni!" Kwa hiyo wakaenda
wakaanza kuua watu mjini kote. 8 [e]Wakati
walikuwa wakiwaua watu, nami nilikuwa
nimeachwa peke yangu, nikaanguka
kifudifudi, nikapiga kelele nikisema, "Ee
BWANA Mwenyezi! Je, utaangamiza mabaki
yote ya Israeli, katika kumwagwa huku kwa
ghadhabu yako juu ya Yerusalemu?"
9 [f]BWANA akanijibu, "Dhambi ya nyumba
ya Israeli na Yuda imekuwa kubwa mno
kupita kiasi, nchi imejaa umwagaji damu
na mjini kumejaa udhalimu. Kwani
wamesema, 'BWANA ameiacha nchi, BWANA
hauoni.' 10 [g]Kwa hiyo sitawahurumia wala
kuwaachilia lakini nitaleta juu ya vichwa
vyao, yale waliyoyatenda."
11 Ndipo mtu yule aliyekuwa amevaa nguo
ya kitani safi na vifaa vya mwandishi akiwa
amevishikilia upande wake mmoja, akarudi
na kutoa taarifa akisema, "Nimefanya kama
ulivyoniagiza."

*Utukufu Unaondoka Hekaluni*

10 [h]Nikatazama, nikaona juu ya ile nafasi
iliyokuwa juu ya vichwa vya wale
makerubi kulikuwa na kitu mfano wa kiti
cha enzi cha yakuti samawi. 2 [i]BWANA
akamwambia mtu yule aliyekuwa amevaa
nguo ya kitani, "Ingia katikati ya yale
Magurudumu yaliyo chini ya makerubi.
Ukaijaze mikono yako makaa ya mawe
ya moto kutoka katikati ya makerubi
na uyatawanye juu ya mji." Nilipokuwa
nikiangalia, akaingia ndani.
3 Basi wale makerubi walikuwa
wamesimama upande wa kusini wa Hekalu
wakati yule mtu alipoingia ndani, wingu
likaujaza ule ukumbi wa ndani. 4 [j]Kisha
utukufu wa BWANA ukainuka kutoka juu
ya wale makerubi ukaenda kwenye kizingiti
cha Hekalu. Wingu likajaza Hekalu, nao
ukumbi ukajawa na mng'ao wa utukufu
wa BWANA. 5 [k]Sauti ya mabawa ya wale
makerubi ingeweza kusikika mpaka kwenye
ukumbi wa nje, kama sauti ya Mungu
Mwenyezi[l] wakati anapoongea.
6 [m]BWANA alipomwamuru yule mtu
aliyevaa nguo za kitani akisema, "Chukua
moto toka katikati ya magurudumu,
kutoka katikati ya makerubi," yule mtu
aliingia ndani akasimama pembeni mwa
gurudumu. 7 [n]Ndipo mmoja wa wale
makerubi akanyoosha mkono wake kwenye
moto uliokuwa katikati yao. Akachukua
baadhi ya moto na kuutia mikononi mwa
yule mtu aliyevaa mavazi ya kitani, naye
akaupokea akatoka nje. 8 [o](Chini ya mabawa

[a]**9:4** Mwa 4:15; 2Kor 1:22; Yer 7:29; Amo 6:6; Za 119:53; Kut 12:7; Yer 25:29
[b]**9:5** Yer 13:14; Eze 5:11; Kut 32:27; Isa 13:18
[c]**9:6** Eze 8:11-16; Yer 25:29; 1Pet 4:17; Yer 7:32; Mwa 4:15; Kut 12:7
[d]**9:7** Eze 6:7
[e]**9:8** Yos 7:6; Hes 14:5; Amo 7:1-6; Eze 11:3; 7:8
[f]**9:9** Za 58:2; Hab 1:4; Ay 22:13; Eze 14:23; Isa 29:15; Eze 22:13
[g]**9:10** Yer 13:14; Eze 22:29; Isa 22:5; Eze 23:49; 8:18; Isa 22:5
[h]**10:1** Kut 23:10; Eze 1:22; Ufu 4:2-3; Mwa 3:24
[i]**10:2** Eze 1:15; 9:2; Ufu 8:5; 2Sam 22:9
[j]**10:4** Kut 24:16; Eze 44:4; 1:28
[k]**10:5** Ay 40:9; Eze 1:24; 3:15
[l]5 Mungu Mwenyezi hapa ni jina la Kiebrania, El-Shaddai (yaani Mungu Mwenye utoshelevu wote).
[m]**10:6** Dan 7:9
[n]**10:7** Eze 5:4
[o]**10:8** Eze 1:8

ya makerubi paliweza kuonekana kitu kilichofanana na mikono ya mwanadamu.)
9 [a]Nikatazama, nikaona magurudumu manne kando ya makerubi, moja kando ya kila kerubi. Magurudumu hayo yalimetameta kama kito cha zabarajadi.
10 Kule kuonekana kwake, yote manne yalifanana kila gurudumu lilikuwa kama linazunguka ndani ya lingine.
11 [b]Yalipozunguka, yalikwenda kokote katika pande nne walikoelekea wale makerubi. Magurudumu hayakugeuka wakati makerubi yalipokwenda. Makerubi walikwenda upande wowote kichwa kilikoelekea pasipo kugeuka walipokuwa
wakienda. 12 [c]Miili yao yote, pamoja na migongo yao, mikono na mabawa yao yote yalikuwa yamejaa macho kabisa kama yalivyokuwa yale magurudumu yao
manne. 13 Nikasikia magurudumu yakiitwa,
"Magurudumu ya kisulisuli." 14 [d]Kila mmoja
wa wale makerubi alikuwa na nyuso nne: Uso mmoja ulikuwa kama vile wa kerubi, uso wa pili ulikuwa wa mwanadamu, uso wa tatu ulikuwa wa simba na uso wa nne ulikuwa wa tai.
15 [e]Kisha makerubi wakapaa juu. Hawa ndio wale viumbe walio hai niliowaona
kando ya Mto Kebari. 16 [f]Wakati makerubi walipokwenda, magurudumu yaliyoko kando yao yalikwenda na wakati makerubi walipotanda mabawa yao wapate kupaa juu kutoka ardhi, magurudumu yale
hayakuondoka pembeni mwao. 17 [g]Makerubi
yaliposimama kimya, nayo pia yalitulia kimya, nao makerubi yalipoinuka juu, magurudumu nayo yaliinuka juu pamoja nao, kwa sababu roho ya vile viumbe hai ilikuwa ndani yake.
18 [h]Kisha utukufu wa BWANA ukaondoka
pale kwenye kizingiti cha Hekalu na kusimama juu ya wale makerubi.
19 [i]Nilipokuwa nikitazama, makerubi yakatanda mabawa yao na kuinuka kutoka ardhini, nao walipokuwa wakienda, yale magurudumu yakaenda pamoja nao. Wakasimama kwenye ingilio la lango la mashariki la nyumba ya BWANA, nao utukufu wa Mungu wa Israeli ukawa juu yao.
20 [j]Hawa walikuwa ndio viumbe hai niliokuwa nimewaona chini ya Mungu wa Israeli kando ya Mto Kebari, nami nikatambua ya kuwa hao walikuwa
makerubi. 21 [k]Kila mmoja alikuwa na nyuso nne, mabawa manne, chini ya mabawa yao kulikuwa na kile kilichoonekana kama
mikono ya mwanadamu. 22 [l]Nyuso zao
zilifanana kama zile nilizokuwa nimeziona kando ya Mto Kebari. Kila mmoja alikwenda mbele moja kwa moja.

*Hukumu Juu Ya Viongozi Wa Israeli*

11 [m]Ndipo Roho akaniinua na kunileta mpaka kwenye lango la nyumba ya BWANA linalotazama upande wa mashariki. Pale kwenye ingilio la lango kulikuwepo wanaume ishirini na watano, nami nikaona miongoni mwao Yaazania mwana wa Azuri na Pelatia mwana wa Benaya, viongozi wa
watu. 2 [n]BWANA akaniambia, "Mwanadamu, hawa ndio wafanyao hila na kutoa mashauri
potovu katika mji huu. 3 [o]Wao husema, 'Je, hivi karibuni hautakuwa wakati wa kujenga nyumba? Mji huu ni chungu cha kupikia,
nasi ndio nyama.' 4 [p]Kwa hiyo toa unabii dhidi yao, tabiri, Ewe mwanadamu."
5 [q]Kisha Roho wa BWANA akaja juu yangu, naye akaniambia niseme: "Hili ndilo BWANA asemalo: Hili ndilo ninyi mnalosema, ee nyumba ya Israeli, lakini

[a]**10:9** Kut 28:20; Eze 1:15-21; 24:6
[b]**10:11** Eze 1:17
[c]**10:12** Ufu 4:6-8; Eze 1:15-21; 24:6
[d]**10:14** 1Fal 7:36; Eze 41:19; Dan 9:21; Ufu 4:7
[e]**10:15** Isa 6:2; Eze 1:3-5; Za 137:1
[f]**10:16** Eze 1:19
[g]**10:17** Eze 1:20-21; 3:13
[h]**10:18** Za 78:60; 18:10; Eze 7:20-22; 1Sam 4:21
[i]**10:19** Eze 11:1-22; 43:4
[j]**10:20** Eze 1:1-8
[k]**10:21** Eze 1:6, 8
[l]**10:22** Eze 1:10, 12
[m]**11:1** Eze 8:16; 43:4-5; 3:12-14; Yer 5:5
[n]**11:2** Isa 29:20; Nah 1:11
[o]**11:3** Yer 1:13; Eze 24:3; 12:22, 27; Mik 3:3
[p]**11:4** Eze 3:4, 17
[q]**11:5** Ebr 4:11; Za 26:2; Yer 17:10

ninajua mnalowaza mioyoni mwenu.
6 [a]Mmewaua watu wengi katika mji huu
na kujaza barabara zake maiti.
7 [b]“Kwa hiyo hili ndilo asemalo BWANA
Mwenyezi: maiti ulizozitupa huko ni nyama
na mji huu ni chungu, lakini nitawaondoa
mtoke huko. 8 [c]Mnaogopa upanga, nao
upanga huo ndio nitakaouleta juu yenu,
asema BWANA Mwenyezi. 9 [d]Nitawaondoa
mtoke katika mji na kuwatia mikononi mwa
wageni nami nitawaadhibu. 10 [e]Mtaanguka
kwa upanga, nami nitatimiza hukumu dhidi
yenu katika mipaka ya Israeli. Ndipo mtajua
kuwa Mimi ndimi BWANA. 11 [f]Mji huu
hautakuwa chungu kwa ajili yenu, wala
hamtakuwa nyama ndani yake. Nitatoa
hukumu dhidi yenu katika mipaka ya
Israeli. 12 [g]Nanyi mtajua ya kuwa Mimi
ndimi BWANA, kwa kuwa hamkufuata
amri zangu wala kuzishika sheria zangu,
bali mmefuata mwenendo wa mataifa
yanayowazunguka.”
13 [h]Basi nilipokuwa ninatoa unabii,
Pelatia mwana wa Benaya akafa. Ndipo
nikaanguka kifudifudi, nikalia kwa sauti
kuu nikasema, “Ee BWANA Mwenyezi! Je
utaangamiza kabisa mabaki ya Israeli?”
14 Neno la BWANA likanijia kusema:
15 [i]“Mwanadamu, ndugu zako, ndugu zako
ambao ni wa uhusiano wa damu na nyumba
yote ya Israeli, ndio wale ambao watu wa
Yerusalemu wamesema, ‘Wako mbali na
BWANA; nchi hii tulipewa sisi kuwa milki
yetu.’

*Ahadi Ya Kurudi Kwa Israeli*

16 [j]“Kwa hiyo sema, ‘Hili ndilo BWANA
Mwenyezi asemalo: Ingawa niliwapeleka
mbali miongoni mwa mataifa na
kuwatawanya katika nchi mbalimbali,
lakini kwa kitambo kidogo mimi nimekuwa
mahali patakatifu kwao katika nchi
walizokwenda.’
17 [k]“Kwa hiyo sema: ‘Hili ndilo BWANA
Mwenyezi asemalo: Nitawakusanyeni
kutoka mataifa na kuwarudisha kutoka
nchi ambazo mmetawanywa, nami
nitawarudishia nchi ya Israeli.’
18 [lm]“Watairudia nchi na kuondoa
vinyago vyote vya upotovu na sanamu
zote za machukizo. 19 [n]Nitawapa moyo
mmoja na kuweka roho mpya ndani yao,
nitaondoa kutoka ndani yao moyo wa
jiwe na kuwapa moyo wa nyama. 20 [o]Kisha
watafuata amri zangu na kuwa waangalifu
kutii sheria zangu. Watakuwa watu wangu
nami nitakuwa Mungu wao. 21 [p]Lakini kwa
wale ambao mioyo yao imeambatana na
vinyago vyao vya upotovu na sanamu
zao za machukizo, nitaleta juu ya vichwa
vyao yale waliyotenda asema BWANA
Mwenyezi.”
22 [q]Ndipo wale makerubi, wenye
magurudumu pembeni mwao, wakakunjua
mabawa yao, nao utukufu wa Mungu wa
Israeli ulikuwa juu yao. 23 [r]Basi utukufu wa
BWANA ukapaa juu kutoka mji, ukatua juu
ya mlima ulio upande wa mashariki ya mji.
24 [s]Roho akaniinua na kunileta mpaka kwa
watu wa uhamisho huko Ukaldayo nikiwa
katika yale maono niliyopewa na Roho wa
Mungu.
Ndipo maono niliyokuwa nimeyaona
yakanitoka, 25 [t]nami nikawaeleza wale watu

[a]**11:6** Eze 7:23; 22:6
[b]**11:7** Mik 3:2-3; Eze 24:3-13; Yer 1:13
[c]**11:8** Mit 10:24; Isa 66:4; Law 26:25; Yer 42:16
[d]**11:9** Za 106:41; Eze 5:8; Kum 28:36
[e]**11:10** Yer 39:6; 2Fal 14:25
[f]**11:11** Eze 24:6
[g]**11:12** Law 18:4; Eze 18:9; 8:10; 6:7
[h]**11:13** Eze 9:8; Amo 7:2
[i]**11:15** Eze 33:24
[j]**11:16** Za 31:20; Isa 8:14; Za 91:9; Isa 4:6
[k]**11:17** Neh 1:9; Yer 24:5-6; 3:18; 31:16; Eze 20:41; 28:25; 34:13
[l]**11:18** Eze 5:11; 37:23
[m]**11:18** Eze 5:11; 37:23
[n]**11:19** Za 86:11; Yer 32:36; Zek 7:12; Yer 24:7; Rum 2:5; 2Kor 3:3; Eze 36:26; 18:31; 2Nya 30:12
[o]**11:20** Za 105:45; Kut 6:7; Ebr 8:10; Yer 11:4; 32:38; Eze 36:26-28
[p]**11:21** Yer 16:11; Eze 16:43; Ebr 3:12; Eze 9:10
[q]**11:22** Eze 9:3; 10:19; Kut 24:16
[r]**11:23** Eze 1:28; 8:4; Zek 14:4; Eze 10:4
[s]**11:24** 2Kor 12:2; Eze 8:3
[t]**11:25** Eze 3:4, 11; Mdo 20:20

wa uhamisho kila kitu BWANA alichokuwa
amenionyesha.

*Kutekwa Kwa Yuda Kwaelezewa*

12 Neno la BWANA likanijia kusema:
2 [a]“Mwanadamu, unaishi miongoni
mwa watu waasi. Wana macho ya kuona,
lakini hawaoni na masikio ya kusikia lakini
hawasikii, kwa kuwa ni watu waasi.
3 [b]“Kwa hiyo, mwanadamu, funga mizigo
yako kwa kwenda uhamishoni tena wakati
wa mchana, wakiwa wanakutazama, toka
nje na uende mahali pengine kutoka hapo
ulipo. Labda wataelewa, ingawa wao ni
nyumba ya kuasi. 4 [c]Wakati wa mchana,
wakiwa wanakutazama, toa nje mizigo
yako iliyofungwa kwa ajili ya kwenda
uhamishoni. Kisha wakati wa jioni,
wakiwa wanakutazama toka nje kama
wale waendao uhamishoni. 5 [d]Wakiwa
wanakutazama, toboa ukuta utolee mizigo
yako hapo. 6 [e]Beba mizigo hiyo begani
mwako wakikuangalia uichukue nje wakati
wa giza la jioni. Funika uso wako ili usione
nchi, kwa maana nimekufanya ishara kwa
nyumba ya Israeli.”
7 [f]Basi nikafanya kama nilivyoamriwa.
Wakati wa mchana nilitoa vitu vyangu
nje vilivyofungwa tayari kwa uhamishoni.
Kisha wakati wa jioni nikatoboa ukuta
kwa mikono yangu. Nikachukua mizigo
yangu nje wakati wa giza la jioni, nikiwa
nimeibeba mabegani mwangu huku
wakinitazama.
8 Asubuhi neno la BWANA likanijia
kusema: 9 [g]“Mwanadamu, je, nyumba ile
ya kuasi ya Israeli haikukuuliza, ‘Unafanya
nini?’
10 [h]“Waambie, ‘Hili ndilo BWANA
Mwenyezi asemalo: Neno hili linamhusu
mkuu aliye katika Yerusalemu na nyumba
yote ya Israeli ambao wako huko.’
11 [i]Waambie, ‘Mimi ndiye ishara kwenu.’
“Kama vile nilivyotenda, basi litatendeka
vivyo hivyo kwao. Watakwenda uhamishoni
kama mateka.
12 [j]“Naye mkuu aliye miongoni mwao
atabeba mizigo yake begani mwake
kwenye giza la jioni na kuondoka na tundu
litatobolewa ukutani kwa ajili yake ili
kupitia hapo. Atafunika uso wake ili kwamba
asiweze kuiona nchi. 13 [k]Nitatandaza wavu
wangu kwa ajili yake, naye atanaswa
kwenye mtego wangu, nitamleta mpaka
Babeli, nchi ya Wakaldayo, lakini hataiona,
naye atafia huko. 14 [l]Wote wanaomzunguka
nitawatawanya pande zote, watumishi wake
na majeshi yake yote, nami nitawafuatilia
kwa upanga uliofutwa.
15 [m]“Wao watajua kwamba Mimi ndimi
BWANA, nitakapowatawanya miongoni
mwa mataifa na kuwafukuza huku na
huko katika nchi zote. 16 [n]Lakini nitawaacha
wachache wao waokoke na upanga, njaa
na tauni, ili kwamba katika mataifa
watakakokwenda waweze kutambua
matendo ya machukizo waliotenda. Ndipo
watajua kuwa Mimi ndimi BWANA.”
17 Neno la BWANA likanijia kusema:
18 [o]“Mwanadamu, tetemeka wakati ulapo
chakula chako, tetemeka kwa hofu wakati
unywapo maji yako. 19 [p]Waambie watu wa
nchi: ‘Hili ndilo BWANA Mwenyezi asemalo
kuhusu hao wanaoishi Yerusalemu na
katika nchi ya Israeli: Watakula chakula
chao kwa wasiwasi na kunywa maji yao
kwa kufadhaika, kwa kuwa nchi yao
itanyang’anywa kila kitu chake kwa sababu

[a]**12:2** Isa 6:10; Mk 8:18; Yer 5:21; Mt 13:15; Za 78:40; Yer 42:21; Mk 4:12
[b]**12:3** Yer 36:3; 26:3; Eze 3:27; 2Tim 2:25-26
[c]**12:4** 2Fal 25:4; Yer 39:4
[d]**12:5** Yer 52:7; Amo 4:3
[e]**12:6** Isa 8:18; 20:3
[f]**12:7** Eze 24:18; 37:10
[g]**12:9** Eze 20:49; 24:19; 7:12
[h]**12:10** Mal 1:1
[i]**12:11** 2Fal 25:7; Yer 15:2; Isa 8:18; Zek 3:8; Yer 52:15
[j]**12:12** Yer 39:4; 52:7
[k]**12:13** Ay 19:6; Eze 32:3; Hos 7:12; Isa 24:17-18; Mao 4:20; Yer 39:7; 24:8; Eze 17:20; 19:8; 17:16
[l]**12:14** Eze 5:10; 2Fal 25:5; Yer 21:7; Eze 17:21
[m]**12:15** Za 9:16; Eze 6:7, 14; 11:10
[n]**12:16** Yer 4:27; 22:8-9; Eze 36:20; 6:8-10; 14:22
[o]**12:18** Mao 5:9; Eze 4:16
[p]**12:19** Yer 10:22; Zek 7:14; Eze 4:16; 6:6-14; Mik 7:13

ya udhalimu wa wote wanaoishi humo.
20 [a]Miji inayokaliwa na watu itaharibiwa
na nchi itakuwa ukiwa. Ndipo mtakapojua
kwamba Mimi ndimi BWANA.' "
21 Neno la BWANA likanijia kusema:
22 [b]"Mwanadamu, ni nini hii mithali mlio
nayo katika nchi ya Israeli: 'Siku zinapita
na hakuna maono yoyote yanayotimia?'
23 [c]Waambie, 'Hili ndilo BWANA Mwenyezi
asemalo: Nitaikomesha mithali hii,
nao hawataitumia tena katika Israeli.'
Waambie, 'Siku zimekaribia wakati kila
maono yatakapotimizwa. 24 [d]Kwa maana
hapatakuwepo tena na maono ya uongo
wala ubashiri wa udanganyifu miongoni
mwa watu wa Israeli. 25 [e]Lakini Mimi
BWANA nitasema neno nitakalo, nalo
litatimizwa bila kuchelewa. Kwa maana
katika siku zako, wewe nyumba ya kuasi,
nitatimiza kila nisemalo, asema BWANA
Mwenyezi.' "
26 Neno la BWANA likanijia kusema:
27 [f]"Mwanadamu, nyumba ya Israeli
inasema, 'Maono yale anayoyaona ni kwa
ajili ya miaka mingi ijayo, naye hutabiri
kuhusu siku zijazo zilizo mbali.'
28 "Kwa hiyo, waambie, 'Hili ndilo
BWANA Mwenyezi asemalo: Hakuna
maneno yangu yatakayocheleweshwa tena
zaidi, lolote nisemalo litatimizwa, asema
BWANA Mwenyezi.' "

*Manabii Wa Uongo Walaumiwa*

13 Neno la BWANA likanijia kusema:
2 [g]"Mwanadamu, tabiri dhidi ya
manabii wa Israeli wanaotabiri sasa.
Waambie hao ambao hutabiri kutokana
na mawazo yao wenyewe: 'Sikia neno la
BWANA! 3 [h]Hili ndilo BWANA Mwenyezi
asemalo: Ole wao manabii wapumbavu
wafuatao roho yao wenyewe na wala
hawajaona chochote! 4 [i]Manabii wako,
ee Israeli, ni kama mbweha katikati ya
magofu. 5 [j]Hamjakwea kwenda kuziba
mahali palipobomoka katika ukuta ili
kuukarabati kwa ajili ya nyumba ya Israeli,
ili kwamba isimame imara kwenye vita
katika siku ya BWANA. 6 [k]Maono yao ni ya
uongo na ubashiri wao ni wa udanganyifu.
Wao husema, "BWANA amesema," wakati
BWANA hakuwatuma, bado wakitarajia
maneno yao kutimizwa. 7 [l]Je, hamjaona
maono ya uongo na kusema ubashiri wa
udanganyifu hapo msemapo, "BWANA
asema," lakini Mimi sijasema?
8 [m]" 'Kwa hiyo hili ndilo BWANA Mwenyezi
asemalo: Kwa sababu ya uongo wa maneno
yenu na kwa madanganyo ya maono yenu,
Mimi ni kinyume na ninyi, asema BWANA
Mwenyezi. 9 [n]Mkono wangu utakuwa
dhidi ya manabii ambao huona maono ya
uongo na kusema ubashiri wa udanganyifu.
Hawatakuwa katika baraza la watu wangu
au kuandikwa katika kumbukumbu ya
nyumba ya Israeli wala hawataingia katika
nchi ya Israeli. Ndipo mtajua kuwa Mimi
ndimi BWANA Mwenyezi.
10 [o]" 'Kwa sababu ni kweli wanapotosha
watu wangu, wakisema, "Amani," wakati
ambapo hakuna amani, pia kwa sababu,
wakati ukuta dhaifu unapojengwa,
wanaufunika kwa kupaka chokaa, 11 [p]kwa
hiyo waambie hao wanaoupaka chokaa
isiyokorogwa vyema kwamba ukuta huo
utaanguka. Mvua kubwa ya mafuriko
itanyesha, nami nitaleta mvua ya mawe

[a]**12:20** Isa 7:23-24; Yer 4:7; 25:9
[b]**12:22** Isa 5:19; 2Pet 3:4; Za 37:13; 49:4; Eze 3:11; Amo 6:3
[c]**12:23** Yoe 2:1; Sef 1:14; Eze 7:7; 18:3; Za 37:13
[d]**12:24** Mik 3:6; Zek 13:2-4; Mao 2:14; Yer 14:14; Eze 13:23
[e]**12:25** Hes 14:28-32; Dan 9:12; Hab 1:5; Hes 11:23; Eze 13:6; Isa 14:24; Yer 15:9
[f]**12:27** Dan 10:14; Mt 24:48-50; Isa 5:19; Eze 11:3
[g]**13:2** Yer 23:16; 37:19; 14:14; Isa 9:15; Yer 28:15; Eze 22:28
[h]**13:3** Mao 2:14; Hos 9:7; Yer 23:25-32
[i]**13:4** Mik 3:5; Wim 2:15; 2Kor 11:13
[j]**13:5** Isa 58:12; Eze 22:30; 7:19; 30:3
[k]**13:6** Yer 28:15; 29:9; 23:16; 14:14; Eze 12:24-25; 22:28
[l]**13:7** Yer 30:10
[m]**13:8** Yer 21:13
[n]**13:9** Kum 32:32; Yer 17:13; Kut 6:2; Ebr 12:23; Yer 20:3-6; Eze 20:38
[o]**13:10** 2Tim 3:13; Yer 50:6; 23:13; Eze 7:25; 22:28; Yer 4:10
[p]**13:11** Eze 38:22; Za 11:6; Yos 10:11; Ay 38:23

inyeshe kwa nguvu, nao upepo wa dhoruba
utavuma juu yake. 12 Wakati ukuta
utakapoanguka, je, watu hawatawauliza,
“Iko wapi chokaa mliyopaka ukuta?”
13 [a]“ ‘Kwa hiyo hili ndilo BWANA
Mwenyezi asemalo: Katika ghadhabu yangu
nitauachia upepo wa dhoruba, pia katika
hasira yangu mvua ya mawe na mvua ya
mafuriko itanyesha ikiwa na ghadhabu
ya kuangamiza. 14 [b]Nitaubomoa ukuta
mlioupaka chokaa na kuuangusha chini ili
msingi wake uachwe wazi. Utakapoanguka,
mtaangamizwa ndani yake, nanyi mtajua
kuwa Mimi ndimi BWANA. 15 Hivyo ndivyo
nitakavyoitimiza ghadhabu yangu dhidi ya
huo ukuta na dhidi yao walioupaka chokaa.
Nitawaambia ninyi, “Ukuta umebomoka
na vivyo hivyo wale walioupaka chokaa,
16 [c]wale manabii wa Israeli waliotabiri juu
ya Yerusalemu na kuona maono ya amani
kwa ajili yake wakati kulipokuwa hakuna
amani, asema BWANA Mwenyezi.” ’
17 [d]“Sasa, mwanadamu, kaza uso wako
dhidi ya binti za watu wako wanaotabiri
mambo kutoka mawazo yao wenyewe.
Tabiri dhidi yao 18 [e]na useme, ‘Hili ndilo
BWANA Mwenyezi asemalo: Ole wao
wanawake washonao hirizi za uchawi juu
ya viwiko vyao vyote na kutengeneza shela
za urefu wa aina mbalimbali kwa ajili ya
kufunika vichwa vyao kwa makusudi ya
kuwanasa watu. Je, mtatega uhai wa watu
wangu lakini ninyi mponye wa kwenu?
19 [f]Ninyi mmeninajisi miongoni mwa watu
wangu kwa ajili ya konzi chache za shayiri
na chembe za mkate. Kwa kuwaambia uongo
watu wangu, wale ambao husikiliza uongo,
mmewaua wale watu ambao wasingekufa
na kuwaacha hai wale ambao wasingeishi.
20 [g]“ ‘Kwa hiyo hili ndilo BWANA
Mwenyezi asemalo: Mimi niko kinyume
na hizo hirizi zenu za uchawi ambazo
kwa hizo mnawatega watu kama ndege,
nami nitazirarua kutoka mikononi mwenu,
nitawaweka huru watu wale mliowatega
kama ndege. 21 [h]Nitazirarua shela zenu na
kuwaokoa watu wangu kutoka mikononi
mwenu, nao hawatakuwa tena mawindo ya
nguvu zenu. Ndipo mtakapojua kuwa Mimi
ndimi BWANA. 22 [i]Kwa sababu mliwavunja
moyo wenye haki kwa uongo wenu, wakati
mimi sikuwaletea huzuni na kwa kuwa
mliwatia moyo waovu ili wasiziache njia
zao mbaya na hivyo kuokoa maisha yao,
23 [j]kwa hiyo hamtaona tena maono ya
uongo wala kufanya ubashiri. Nitawaokoa
watu wangu kutoka mikononi mwenu.
Nanyi ndipo mtakapojua kuwa Mimi ndimi
BWANA.’ ”

### *Waabudu Sanamu Walaumiwa*

14 [k]Baadhi ya wazee wa Israeli walinijia
na kuketi mbele yangu. 2 Ndipo neno la
BWANA likanijia kusema: 3 [l]“Mwanadamu,
watu hawa wameweka sanamu katika
mioyo yao na kuweka vitu viovu vya
kukwaza mbele ya macho yao. Je, kweli
niwaruhusu waniulize jambo lolote?
4 Kwa hiyo sema nao uwaambie, ‘Hili
ndilo BWANA Mwenyezi asemalo: Wakati
Mwisraeli yeyote anapoweka sanamu
moyoni mwake na kuweka kitu kiovu cha
kukwaza mbele ya macho yake na kisha
akaenda kwa nabii, Mimi BWANA nitamjibu
peke yangu sawasawa na ukubwa wa ibada
yake ya sanamu. 5 [m]Nitafanya jambo hili ili
kukamata tena mioyo ya watu wa Israeli,
ambao wote wameniacha kwa ajili ya
sanamu zao.’

---

[a]**13:13** Yos 10:11; Ufu 11:19; Kut 9:25; Ay 38:23; Ufu 16:21; Isa 30:30
[b]**13:14** Mik 1:6; Yer 6:15; Eze 14:8; Isa 22:5
[c]**13:16** Isa 57:21; Yer 6:14; 8:11; Eze 7:25
[d]**13:17** Kut 15:20; Ufu 2:20; Isa 3:16; Eze 4:7; 25:2; 28:21
[e]**13:18** 2Pet 2:14
[f]**13:19** Yer 44:26; Eze 22:26; 20:39; Mit 28:21; Mik 3:11; Rum 14:15
[g]**13:20** Za 124:7
[h]**13:21** Za 91:3
[i]**13:22** Yer 23:14; Eze 18:21; Mit 19:27; Isa 9:21; Eze 33:14-16
[j]**13:23** Eze 12:24; Mik 3:6; Eze 14:8; Neh 6:12; Za 72:14
[k]**14:1** Eze 8:1; 20:1
[l]**14:3** Eze 7:19; Ufu 2:14; Isa 1:15; Eze 20:31; Mit 15:8; Eze 6:4
[m]**14:5** Ebr 3:12-19; Kum 32:15; Hos 5:7; Yer 2:11; Eze 16:45; Zek 11:8

6 [a]“Kwa hiyo iambie nyumba ya Israeli,
‘Hili ndilo BWANA Mwenyezi asemalo:
Tubuni! Geukeni kutoka kwenye sanamu
zenu na mkatae matendo yenu yote ya
machukizo!
7 [b]“ ‘Mwisraeli yeyote au mgeni yeyote
anayeishi katika Israeli anapojitenga nami
na kujiwekea sanamu katika moyo wake
na kwa hivyo kuweka kitu kiovu cha
kukwaza mbele ya macho yake na kisha
akamwendea nabii kuuliza shauri kwangu,
mimi BWANA nitamjibu mwenyewe.
8 [c]Nitaukaza uso wangu dhidi ya mtu huyo
na kumwadhibu na kumfanya ishara kwa
watu. Nitamkatilia mbali kutoka watu
wangu. Ndipo mtakapojua kuwa Mimi
ndimi BWANA.
9 [d]“ ‘Naye nabii kama atakuwa
ameshawishika kutoa unabii, Mimi BWANA
nitakuwa nimemshawishi nabii huyo, nami
nitaunyoosha mkono wangu dhidi yake
na kumwangamiza kutoka miongoni mwa
watu wangu Israeli. 10 Watachukua hatia
yao, nabii atakuwa na hatia sawa na yule
mtu aliyekuja kuuliza neno kwake.
11 [e]“ ‘Ndipo watu wa Israeli hawataniacha
tena, wala kujitia unajisi tena kwa dhambi
zao zote. Ndipo watakuwa watu wangu
nami nitakuwa Mungu wao, asema BWANA
Mwenyezi.’ ”

*Hukumu Isiyoepukika*

12 Neno la BWANA likanijia kusema,
13 [f]“Mwanadamu, kama nchi itanitenda
dhambi kwa kutokuwa waaminifu nami
nikinyoosha mkono wangu dhidi yake
kukatilia mbali upatikanaji wake wa
chakula na kuipelekea njaa na kuua watu
wake na wanyama wao, 14 [g]hata kama
watu hawa watatu: Noa, Danieli na Ayubu
wangekuwa ndani ya nchi hiyo, ndio hao tu
wangeweza kujiokoa wenyewe kwa uadilifu
wao, asema BWANA Mwenyezi.
15 [h]“Au kama nikipeleka wanyama pori
katika nchi hiyo yote na kuifanya isiwe na
watoto, nayo ikawa ukiwa kwamba hakuna
mtu apitaye katika nchi hiyo kwa sababu ya
wanyama pori, 16 [i]hakika kama niishivyo,
asema BWANA Mwenyezi, hata kama watu
hawa watatu wangekuwa humo ndani yake,
wasingeweza kuokoa wana wao wala binti
zao. Wao peke yao wangeokolewa, lakini
nchi ingekuwa ukiwa.
17 [j]“Au kama nikileta upanga dhidi ya
nchi hiyo na kusema, ‘Upanga na upite
katika nchi yote,’ nami nikiua watu wake na
wanyama wao, 18 [k]hakika kama niishivyo,
asema BWANA Mwenyezi, hata kama watu
hawa watatu wangekuwa humo ndani yake,
wasingeweza kuokoa wana wao wala binti
zao. Wao wenyewe tu wangeokolewa.
19 [l]“Au kama nikipeleka tauni katika nchi
hiyo na kumwaga ghadhabu yangu juu yake
kwa njia ya kumwaga damu, kuua watu
wake na wanyama wao, 20 [m]hakika kama
niishivyo, asema BWANA Mwenyezi, hata
kama Noa, Danieli na Ayubu wangekuwa
humo ndani yake, wasingeweza kumwokoa
mwana wala binti. Wao wangeweza
kujiokoa wenyewe tu kwa uadilifu wao.
21 [n]“Kwa maana hili ndilo BWANA
Mwenyezi asemalo: Itakuwa vibaya kiasi
gani nitakapopeleka dhidi ya Yerusalemu
hukumu zangu nne za kutisha, yaani,
upanga, njaa, wanyama pori na tauni,
ili kuua watu wake na wanyama wao!

[a]**14:6** Isa 2:20; 30:22; Neh 1:9; Yer 3:12; 35:15
[b]**14:7** Kut 12:48; 20:10; Mt 6:24; Yer 2:13; Isa 8:14; Mwa 25:22; Hos 4:5
[c]**14:8** Eze 15:7; Za 102:8; Hes 26:10; Eze 5:15; Yer 42:20; Hes 16:38
[d]**14:9** Yer 14:15; Isa 63:17; Yer 4:10; 2Nya 18:22; Zek 13:3; 1Fal 22:23
[e]**14:11** Eze 48:11; 11:19-20; 37:23; Isa 13:19; 51:16
[f]**14:13** Law 26:26; Eze 5:16; 5:16; 6:14; Mit 13:21; Eze 15:8
[g]**14:14** Mwa 6:8-9; Dan 6:13; Ay 42:9; Eze 28:3; 18:20; 3:19
[h]**14:15** Hes 21:6; Eze 5:17; Law 26:22
[i]**14:16** Mwa 19:29; Eze 18:20
[j]**14:17** Law 26:25; Yer 25:27; Eze 25:13; 5:12; Yer 42:16
[k]**14:18** Eze 14:14
[l]**14:19** Yer 14:12; Eze 38:22; Ufu 16:3-6; Eze 7:8; Isa 34:3
[m]**14:20** Eze 14:14
[n]**14:21** Eze 5:17; Amo 4:6-10; Ufu 6:8; Hes 33:4; Isa 31:8; 34:6; Eze 21:3; 2Sam 24:13

22 [a]Lakini watakuwepo wenye kuokoka,
wana na binti wataletwa kutoka nje
ya nchi hiyo. Watawajia ninyi, nanyi
mtakapoona mwenendo wao na matendo
yao, mtafarijika kuhusu maafa niliyoleta
juu ya Yerusalemu, kwa ajili ya yale yote
niliyoleta juu yake. 23 [b]Mtafarijika wakati
mtakapoona mwenendo wao na matendo
yao, kwa kuwa mtajua kwamba sikufanya
lolote ndani yake bila sababu, asema
BWANA Mwenyezi."

*Yerusalemu Mzabibu Usiofaa*

15 Neno la BWANA likanijia kusema:
2 [c]"Mwanadamu, je, ni vipi mti
wa mzabibu unaweza kuwa bora zaidi
kuliko tawi la mti mwingine wowote
ndani ya msitu? 3 [d]Je, mti wake kamwe
huchukuliwa na kutengeneza chochote
cha manufaa? Je, watu hutengeneza vigingi
vya kuning'inizia vitu kutokana na huo
mti wake? 4 [e]Nao baada ya kutiwa motoni
kama nishati na moto ukateketeza ncha
zote mbili na kuunguza sehemu ya kati,
je, unafaa kwa lolote? 5 Kama haukufaa
kitu chochote ulipokuwa mzima, je, si
zaidi sana sasa ambapo hauwezekani
kufanyishwa chochote cha kufaa baada ya
moto kuuchoma na kuuunguza?

6 "Kwa hiyo hili ndilo BWANA Mwenyezi
asemalo: Kama nilivyoutoa mti wa
mzabibu miongoni mwa miti ya msituni
kuwa nishati kwa ajili ya moto, hivyo
ndivyo nitakavyowatendea watu waishio
Yerusalemu. 7 [f]Nitaukaza uso wangu
dhidi yao. Ingawa watakuwa wameokoka
kwenye moto, bado moto utawateketeza.
Nami nitakapoukaza uso wangu dhidi yao,
ninyi mtajua kwamba Mimi ndimi BWANA.
8 [g]Nitaifanya nchi kuwa ukiwa kwa sababu
wamekuwa si waaminifu, asema BWANA
Mwenyezi."

*Yerusalemu, Mwanamke Asiye Mwaminifu*

16 Neno la BWANA likanijia kusema:
2 [h]"Mwanadamu, ijulishe Yerusalemu
kuhusu mwenendo wake wa machukizo
3 [i]na useme, 'Hili ndilo BWANA Mwenyezi,
analomwambia Yerusalemu: Wewe asili
yako na kuzaliwa kwako ni katika nchi
ya Kanaani, baba yako alikuwa Mwamori,
naye mama yako alikuwa Mhiti. 4 [j]Siku
uliyozaliwa kitovu chako hakikukatwa,
wala hukuogeshwa kwa maji ili kukufanya
safi, wala hukusuguliwa kwa chumvi wala
kufunikwa kwa nguo. 5 Hakuna yeyote
aliyekuonea huruma au kukusikitikia kiasi
cha kukutendea mojawapo ya mambo
haya. Badala yake, ulipozaliwa ulitupwa
nje penye uwanja, kwa kuwa katika siku
uliyozaliwa ulidharauliwa.

6 [k]" 'Ndipo nilipopita karibu nawe
nikakuona ukigaagaa kwenye damu yako,
nawe ulipokuwa umelala hapo penye hiyo
damu nikakuambia, "Ishi!" 7 [l]Nilikufanya
uote kama mmea wa shambani. Ukakua na
kuongezeka sana, ukawa kito cha thamani
kuliko vyote. Matiti yako yakatokeza na
nywele zako zikaota, wewe uliyekuwa uchi
na bila kitu chochote.

8 [m]" 'Baadaye nikapita karibu nawe,
nilipokutazama na kukuona kuwa umefikia
umri wa kupendwa, nililitandaza vazi
langu juu yako na kuufunika uchi wako.
Nikakuapia na kuingia kwenye Agano na
wewe, asema BWANA Mwenyezi, nawe
ukawa wangu.

9 [n]" 'Nilikuogesha kwa maji, nikakuosha ile
damu na kukupaka mafuta. 10 [o]Nikakuvika

---

[a]**14:22** Eze 12:16; 20:43; Yer 41:16; Eze 31:16; 32:31
[b]**14:23** Yer 22:8-9; Eze 8:6-18
[c]**15:2** Za 80:8-16; Yn 15:2; Yer 2:21; Isa 27:2-6; 5:1-7; Hos 10:1
[d]**15:3** Yer 13:10; Isa 22:23
[e]**15:4** Eze 17:3-10; Yn 15:6; Eze 19:14
[f]**15:7** Yer 21:10; Law 26:17; Za 34:16; Isa 24:18; Amo 9:1-4; Eze 14:8; 5:2-4
[g]**15:8** Eze 14:13; 17:20; Amo 5:19; Eze 18:24
[h]**16:2** Eze 20:4; 8:17; 22:2; 23:36; Isa 57:12
[i]**16:3** Mwa 11:25-29; Eze 21:30; Mwa 10:15; Yos 24:14-15; Mwa 12:18; 16:15
[j]**16:4** Hos 2:3
[k]**16:6** Kut 19:4; Eze 18:23, 32
[l]**16:7** Kum 1:10; Kut 1:7
[m]**16:8** Rut 3:9; Kut 19:5; Hos 2:7-20; Mal 2:4; Yer 2:2; 11:10
[n]**16:9** Rut 3:3
[o]**16:10** Kut 26:36; Isa 19:9; Eze 27:16; Isa 3:23

vazi lililotariziwa na kukuvalisha viatu
vya kamba vya ngozi. Nikakuvika nguo
za kitani safi na kukufunika kwa mavazi
ya thamani kubwa. 11 [a]Nikakupamba kwa
vito: nikakuvika bangili mikononi mwako
na mkufu shingoni mwako, 12 [b]nikaweka
hazama puani mwako, vipuli masikioni
mwako na taji nzuri sana kichwani mwako.
13 [c]Kwa hiyo ulipambwa kwa dhahabu na
fedha, nguo zako zilikuwa za kitani safi,
hariri na nguo iliyokuwa imetariziwa.
Chakula chako kilikuwa unga laini, asali
na mafuta ya zeituni. Ukawa mzuri sana
ukainuka kuwa malkia. 14 [d]Umaarufu
wako ulifahamika miongoni mwa mataifa
kwa ajili ya uzuri wako, kwani ulikuwa
mkamilifu kwa ajili ya utukufu wangu
niliokuwa nimeuweka juu yako, asema
BWANA Mwenyezi.

15 [e]" 'Lakini ulitumainia uzuri wako na
kutumia umaarufu wako kuwa kahaba.
Ulifanya uzinzi kwa kila mtu aliyepita, uzuri
wako ukawa kwa ajili yake. 16 [f]Ulichukua
baadhi ya mavazi yako ukayatumia
kupamba mahali pako pa juu pa kuabudia
miungu, mahali ambapo ulifanyia ukahaba
wako. Mambo ya namna hiyo hayastahili
kutendeka wala kamwe kutokea. 17 [g]Pia
ulichukua vito vizuri nilivyokupa, vito
vilivyotengenezwa kwa dhahabu yangu
na fedha yangu, ukajitengenezea navyo
sanamu za kiume na ukafanya ukahaba
nazo. 18 [h]Ukayachukua mavazi yako
niliyokupa yaliyotariziwa na ukazivalisha
hizo sanamu, ukatoa mbele ya hizo sanamu
mafuta yangu na uvumba wangu. 19 [i]Pia
chakula changu nilichokupa ili ule: unga
laini, mafuta ya zeituni na asali, ulivitoa
mbele yao kuwa uvumba wa harufu nzuri.
Hayo ndiyo yaliyotokea, asema BWANA
Mwenyezi.

20 [j]" 'Nawe uliwachukua wanao na binti
zako ulionizalia mimi na kuwatoa kafara
kuwa chakula kwa sanamu. Je, ukahaba
wako haukukutosha? 21 [k]Uliwachinja watoto
wangu na kuwatoa kafara kwa sanamu.
22 [l]Katika matendo yako yote ya machukizo,
pamoja na ukahaba wako hukukumbuka
siku za ujana wako, wakati ulipokuwa
uchi kabisa bila kitu chochote, ulipokuwa
ukigaagaa kwenye damu yako.

23 [m]" 'Ole! Ole wako! Asema BWANA
Mwenyezi. Pamoja na maovu yako yote
mengine, 24 [n]Ukajijengea jukwaa na
kujifanyia mahali pa fahari pa ibada za
miungu kwenye kila uwanja wa mikutano.
25 [o]Katika kila mwanzo wa barabara ulijenga
mahali pa fahari pa ibada za miungu na
kuaibisha uzuri wako, ukiutoa mwili wako
kwa kuzidisha uzinzi kwa kila apitaye.
26 [p]Ulifanya ukahaba wako na Wamisri,
jirani zako waliojaa tamaa, ukaichochea
hasira yangu kwa kuongezeka kwa uzinzi
wako. 27 [q]Hivyo nilinyoosha mkono wangu
dhidi yako na kuipunguza nchi yako,
nikakutia kwenye ulafi wa adui zako,
binti za Wafilisti, walioshtushwa na tabia
yako ya uasherati. 28 [r]Ulifanya ukahaba na
Waashuru pia, kwa kuwa hukuridhika, hata
baada ya hayo, ukawa bado hukutosheleka.
29 [s]Ndipo ukaongeza uzinzi wako kwa
Wakaldayo nchi ya wafanyabiashara, hata
katika hili hukutosheka.

---

[a]**16:11** Yer 4:30; Eze 23:40; Isa 3:19; Eze 23:42; Mwa 41:42; Za 73:6
[b]**16:12** Isa 3:21; 28:5; Yer 13:18; Mwa 35:4
[c]**16:13** 1Sam 10:1; 1Fal 4:21; Es 2:9, 17; Za 48:2; Es 5:1; Kum 32:13-14
[d]**16:14** 1Fal 10:24; Es 1:11; Za 48:2; Mao 2:15; Eze 5:5
[e]**16:15** Yer 2:20; Isa 57:8; Mik 3:11; Eze 23:3; 27:3
[f]**16:16** 2Fal 23:7; Hos 2:8; Isa 57:7
[g]**16:17** Eze 7:20; Hos 2:13
[h]**16:18** Yer 44:5
[i]**16:19** Isa 57:7; Yer 44:21; Za 78:58; Hos 2:8
[j]**16:20** Yer 7:31; Kut 13:2; Za 106:37-38; Isa 57:5; Eze 23:37
[k]**16:21** 2Fal 17:17; Yer 19:5
[l]**16:22** Za 25:7; Hos 11:1; Za 88:15; Hos 2:15; Yer 2:2
[m]**16:23** Eze 24:6
[n]**16:24** Za 78:58; Yer 44:21; Isa 57:7; Eze 20:28; Yer 2:20; 3:2
[o]**16:25** Mit 9:14; Yer 6:15; 3:2
[p]**16:26** 1Fal 14:9; Eze 8:17; Yer 11:15; Isa 57:8; 23:17; Eze 23:17; 33:19-21; 20:8
[q]**16:27** Eze 20:33; 25:13; 2Nya 28:18; Yer 34:20
[r]**16:28** 2Fal 16:7; Amu 10:6; Eze 23:14; Isa 57:8
[s]**16:29** Yer 3:1; Eze 23:14-17; Nah 3:4

30 [a]“ ‘Tazama jinsi ulivyo na dhamiri
dhaifu, asema BWANA Mwenyezi,
unapofanya mambo haya yote, ukifanya
kama kahaba asiyekuwa na aibu!
31 [b]Unapojenga jukwaa lako kila mwanzo
wa barabara na kufanyiza mahali pa fahari
pa ibada za miungu katika kila kiwanja cha
wazi, lakini hukuwa kama kahaba, kwa
sababu ulidharau malipo.
32 “ ‘Wewe mke mzinzi! Unapenda
wageni, kuliko mume wako mwenyewe.
33 [c]Kila kahaba hupokea malipo, lakini wewe
hutoa zawadi kwa wapenzi wako wote,
ukiwahonga ili waje kwako kutoka kila
mahali kwa ajili ya ukahaba wako. 34 Kwa
hiyo wewe ulikuwa tofauti na wanawake
wengine kwenye ukahaba wako, hakuna
aliyekutongoza ili kuzini naye, wewe ndiye
uliyelipa wakati hakuna malipo uliyolipwa
wewe. Wewe ulikuwa tofauti.
35 “ ‘Kwa hiyo, wewe kahaba, sikia neno
la BWANA! 36 [d]Hili ndilo BWANA Mwenyezi
asemalo: Kwa kuwa umemwaga tamaa
zako na kuonyesha uchi wako katika
uzinzi wako kwa wapenzi wako na kwa
sababu ya sanamu zako zote za machukizo
na kwa sababu uliwapa damu ya watoto
wako, 37 [e]kwa hiyo nitawakusanya wapenzi
wako wote, wale ambao ulijifurahisha nao,
wale uliowapenda na wale uliowachukia
pia. Nitawakusanya wote dhidi yako
kutoka pande zote na nitakuvua nguo
mbele yao, nao wataona uchi wako wote.
38 [f]Nitakuhukumia adhabu wanayopewa
wanawake wafanyao uasherati na hao
wamwagao damu, nitaleta juu yenu kisasi
cha damu cha ghadhabu yangu na wivu wa
hasira yangu. 39 [g]Kisha nitakutia mikononi
mwa wapenzi wako, nao watabomoa
majukwaa yako na kuharibu mahali pako
pa fahari pa ibada ya miungu. Watakuvua
nguo zako na kuchukua vito vyako vya
thamani na kukuacha uchi na bila kitu.
40 [h]Wataleta kundi la watu dhidi yako,
watakaokupiga kwa mawe na kukukatakata
vipande vipande kwa panga zao.
41 [i]Watachoma nyumba zako na kutekeleza
adhabu juu yako machoni pa wanawake
wengi. Nitakomesha ukahaba wako, nawe
hutawalipa tena wapenzi wako. 42 [j]Ndipo
ghadhabu yangu dhidi yako itakapopungua
na wivu wa hasira yangu utaondoka kwako.
Nitatulia wala sitakasirika tena.
43 [k]“ ‘Kwa sababu hukuzikumbuka siku
za ujana wako, lakini ulinikasirisha kwa
mambo haya yote, hakika nitaleta juu
ya kichwa chako yale uliyotenda, asema
BWANA Mwenyezi. Je hukuongeza uasherati
juu ya matendo yako yote ya kuchukiza?
44 [l]“ ‘Kila mtu atumiaye maneno ya
mithali hii, atayatumia juu yako: “Alivyo
mama, ndivyo alivyo bintiye.” 45 [m]Wewe
ni binti halisi wa mama yako, ambaye
alimchukia kabisa mume wake na watoto
wake, tena wewe ni dada halisi wa dada
zako, waliowachukia kabisa waume zao na
watoto wao. Mama yako alikuwa Mhiti na
baba yako alikuwa Mwamori. 46 [n]Dada yako
mkubwa alikuwa Samaria, aliyeishi upande
wako wa kaskazini na binti zake, pamoja
na dada yake, naye dada yako mdogo,
aliyeishi kusini yako pamoja na binti zake,
alikuwa Sodoma. 47 [o]Hukuziendea njia zao
tu na kuiga matendo yao ya kuchukiza,
bali kwa muda mfupi katika njia zako zote
uliharibika tabia zaidi kuliko wao. 48 [p]Hakika
kama niishivyo, asema BWANA Mwenyezi,
dada yako Sodoma pamoja na binti zake,

---

[a]**16:30** Yer 3:3
[b]**16:31** Eze 16:24, 39
[c]**16:33** Isa 30:6; 57:6; Hos 8:9-10; Mwa 30:15
[d]**16:36** Yer 19:5; Eze 23:10; Yer 2:34
[e]**16:37** Isa 47:2-3; Hos 2:10; Ufu 17:16; Eze 23:9; Yer 13:22; Hos 8:10
[f]**16:38** Mwa 38:24; Eze 23:25; Law 20:10; Za 79:3-5; Kut 21:12; Sef 1:17
[g]**16:39** Eze 23:26; Hos 2:3; Eze 21:31; 2Fal 18:11
[h]**16:40** Yn 8:5-7
[i]**16:41** Kum 13:16; Yer 19:13; Eze 23:10; 22:15; Rum 2:8; Eze 23:48
[j]**16:42** 2Sam 24:25; Eze 5:13; Isa 40:1-2; 54:9
[k]**16:43** Kut 15:24; Za 78:42; Eze 11:21; 22:31
[l]**16:44** Za 49:4
[m]**16:45** Eze 14:5; 23:5; Yer 44:19
[n]**16:46** Mwa 13:10-13; Ufu 11:8; Mwa 18:20; Yer 3:8-11; Eze 23:4
[o]**16:47** 2Fal 21:9; Eze 5:6-7
[p]**16:48** Mt 10:15; 11:23-24; Lk 10:12; Mwa 15:2; 19:25

kamwe hawakufanya yale ambayo wewe
na binti zako mmefanya.
49 [a]“ ‘Sasa hii ilikuwa ndiyo dhambi ya
dada yako Sodoma: yeye na binti zake
walikuwa na majivuno, walafi na wazembe,
hawakuwasaidia maskini na wahitaji.
50 [b]Walijivuna na kufanya mambo ya
machukizo sana mbele zangu. Kwa hiyo
niliwakatilia mbali nami kama mlivyoona.
51 [c]Samaria hakufanya hata nusu ya dhambi
ulizofanya. Wewe umefanya mambo mengi
sana ya kuchukiza kuwaliko wao, nawe
umewafanya dada zako waonekane kama
wenye haki kwa ajili ya mambo haya yote
uliyoyafanya. 52 [d]Chukua aibu yako, kwa
kuwa umefanya uovu wa dada zako uwe
si kitu, nao waonekane kama wenye haki.
Kwa kuwa dhambi zako zilikuwa mbaya
zaidi kuliko zao, wameonekana wenye haki
zaidi kuliko wewe. Kwa hiyo basi, chukua
aibu yako, kwa kuwa umewafanya dada
zako waonekane wenye haki.
53 [e]“ ‘Lakini nitarudisha baraka za
Sodoma na binti zake na za Samaria na
binti zake, nami nitarudisha baraka zako
pamoja na zao, 54 [f]ili upate kuchukua aibu
yako na kufedheheka kwa ajili ya yote
uliyotenda ambayo yamekuwa faraja kwao
wakijilinganisha na wewe. 55 [g]Nao dada
zako, Sodoma na binti zake na Samaria
na binti zake, watarudishwa kama vile
walivyokuwa mwanzoni, nawe pamoja na
binti zako mtarudishwa kama mlivyokuwa
hapo awali. 56 Hukuweza hata kumtaja
dada yako Sodoma kwa sababu ya dharau
yako katika siku za kiburi chako, 57 [h]kabla
uovu wako haujafunuliwa. Hata hivyo,
sasa unadhihakiwa na binti za Edomu na
jirani zake wote, na binti za Wafilisti, wale
wote wanaokuzunguka wanakudharau.
58 [i]Utachukua matokeo ya uasherati wako
na matendo yako ya kuchukiza, asema
BWANA.
59 [j]“ ‘Hili ndilo BWANA Mwenyezi asemalo:
Nitakushughulikia kama unavyostahili,
kwa kuwa umedharau kiapo changu kwa
kuvunja Agano. 60 [k]Lakini nitakumbuka
Agano nililolifanya nawe wakati wa ujana
wako, nami nitaweka nawe Agano imara
la milele. 61 [l]Ndipo utakapozikumbuka
njia zako na kuona aibu utakapowapokea
dada zako, wale walio wakubwa wako na
wadogo wako. Nitakupa hao wawe binti
zako, lakini si katika msingi wa Agano
langu na wewe. 62 [m]Hivyo nitalifanya imara
Agano langu na wewe, nawe utajua kuwa
Mimi ndimi BWANA. 63 [n]Basi, nitakapofanya
upatanisho kwa ajili yako, kwa yale yote
uliyoyatenda, utakumbuka na kuaibika,
nawe kamwe hutafumbua tena kinywa
chako kwa sababu ya aibu yako, asema
BWANA Mwenyezi.’ ”

*Tai Wawili Na Mizabibu*

17 [o]Neno la BWANA likanijia kusema:
2 [p]“Mwanadamu, tega kitendawili,
ukawaambie nyumba ya Israeli fumbo.
3 [q]Waambie hivi, ‘Hili ndilo BWANA
Mwenyezi asemalo: Tai mkubwa mwenye
mabawa yenye nguvu, yaliyojaa manyoya
marefu ya rangi mbalimbali, alikuja
Lebanoni. Akatua kwenye kilele cha
mwerezi, 4 [r]akakwanyua ncha yake na
kuichukua mpaka nchi ya wafanyabiashara,
akaipanda huko katika mji wa wachuuzi.

[a]**16:49** Isa 1:10; Mwa 13:13; Eze 28:2; Amo 6:4-8; Yak 5:5; Lk 12:16-20
[b]**16:50** Mwa 18:20-21; Ay 18:18; Mwa 19:5; Za 18:27
[c]**16:51** Yer 3:9-11; Eze 23:11; Mt 12:40-41; Eze 5:6-7
[d]**16:52** Yer 3:11; Eze 23:35
[e]**16:53** Kum 30:3; Yer 48:47; Rum 9:23; Isa 19:24-25; Eze 39:25
[f]**16:54** Yer 2:26; Eze 14:22-23
[g]**16:55** Eze 36:11; Mal 3:4
[h]**16:57** 2Fal 16:6; 2Nya 28:18; Za 137:3
[i]**16:58** Eze 23:49
[j]**16:59** Eze 17:19; Kum 29:12-14
[k]**16:60** Mwa 9:16; Yer 32:40; Kut 2:24; Hos 2:15; Mwa 6:18; Za 25:7
[l]**16:61** Eze 43:10; 44:13; Wim 8:8; Gal 4:26; Eze 20:43; Isa 43:6
[m]**16:62** Hos 2:19-20; Yer 24:7; Ebr 8:6-13; Eze 20:37, 43-44; Kum 29:14; Eze 34:25
[n]**16:63** Rum 3:9; Za 79:9; 78:38; 39:9; Dan 9:7-8; Za 65:3
[o]**17:1** Amu 14:12; Eze 20:49
[p]**17:2** Amu 14:12; Eze 20:49
[q]**17:3** Kum 28:49; Dan 7:4; Yer 22:23; 49:22; Hos 8:1
[r]**17:4** Isa 10:33

5 [a]“ ‘Akachukua baadhi ya mbegu za nchi
yako na kuziweka katika udongo wenye
rutuba. Akazipanda kama mti umeao
kando ya maji mengi, 6 [b]nazo zikaota na
kuwa mzabibu mfupi, unaoeneza matawi
yake. Matawi yake yakamwelekea huyo tai,
mizizi yake ikabaki chini ya huo mzabibu.
Kwa hiyo ukawa mzabibu na kutoa matawi
na vitawi vyenye majani mengi.
7 [c]“ ‘Lakini kulikuwa na tai mwingine
mkubwa, mwenye mabawa yenye nguvu
yaliyojaa manyoya. Tazama! Huu mzabibu
ukatoa mizizi yake kumwelekea huyo tai
kutoka mle kwenye shamba lile ulikopandwa
na kutanda matawi yake kumwelekea kwa
ajili ya kupata maji. 8 [d]Ulikuwa umepandwa
katika udongo mzuri wenye maji mengi ili
uweze kutoa matawi, kuzaa matunda na
uweze kuwa mzabibu mzuri sana.’
9 [e]“Waambie, ‘Hili ndilo Bwana
Mwenyezi asemalo: Je, utastawi? Je,
hautang’olewa na kuondolewa matunda
yake, ili uweze kunyauka? Majani yake
mapya yanayochipua yote yatanyauka.
Hautahitaji mkono wenye nguvu au watu
wengi kuung’oa na mizizi yake. 10 [f]Hata
kama utapandwa pengine, Je, utastawi?
Je, hautanyauka kabisa wakati upepo
wa mashariki utakapoupiga, yaani,
hautanyauka kabisa katika udongo mzuri
ambamo ulikuwa umestawi vizuri?’ ”
11 Ndipo neno la Bwana likanijia
kusema: 12 [g]“Waambie nyumba hii ya
kuasi, ‘Je, mnajua hii ina maana gani?’
Waambie: ‘Mfalme wa Babeli alikwenda
Yerusalemu na kumchukua mfalme na watu
maarufu, akarudi nao na kuwaleta mpaka
Babeli. 13 [h]Ndipo akamchukua mmoja wa
jamaa ya mfalme na kufanya mapatano
naye, akamfanya aape. Akawachukua
pia viongozi wa nchi, 14 [i]ili kuudhoofisha
ufalme huo, usiweze kuinuka tena, ila
uweze kuendelea tu chini ya mapatano
yake. 15 [j]Lakini mfalme aliasi dhidi yake
kwa kutuma wajumbe wake kwenda
Misri ili kupatiwa farasi na jeshi kubwa.
Je, atashinda? Je, atafanikiwa? Je, mtu
afanyaye mambo kama hayo ataokoka?
Je, atavunja mapatano na bado aokoke?
16 [k]“ ‘Hakika kama niishivyo, asema
Bwana Mwenyezi, atafia huko Babeli,
katika nchi ya mfalme aliyemketisha
katika kiti cha enzi, ambaye alidharau
kiapo chake na kuvunja mapatano yake.
17 [l]Farao na jeshi lake kubwa, na wingi wake
wa watu hawataweza kusaidia chochote
katika vita, wakati watakapozungukwa na
jeshi ili kukatilia mbali maisha ya watu
wengi. 18 [m]Alidharau kiapo kwa kuvunja
Agano. Kwa sababu aliahidi kwa mkono
wake mwenyewe na bado akafanya mambo
haya yote, hataokoka.
19 [n]“ ‘Kwa hiyo hili ndilo Bwana
Mwenyezi asemalo: Hakika kama niishivyo,
nitaleta juu ya kichwa chake kiapo
changu, alichokidharau na Agano langu
lile alilolivunja. 20 [o]Nitautandaza wavu
wangu kwa ajili yake, naye atanaswa katika
mtego wangu. Nitamleta mpaka Babeli na
kutekeleza hukumu juu yake huko kwa kuwa
hakuwa mwaminifu kwangu. 21 [p]Askari
wake wote wanaotoroka wataanguka
kwa upanga, nao watakaonusurika
watatawanyika katika pande zote za dunia.
Ndipo utakapojua kuwa Mimi Bwana
nimesema.

---

[a]**17:5** Kum 8:7-9; Isa 15:7; Eze 31:5; Isa 44:5
[b]**17:6** Isa 18:5; Ay 5:3
[c]**17:7** Eze 31:4
[d]**17:8** Ay 18:19; Mal 4:1
[e]**17:9** Yer 42:10; Amo 2:9
[f]**17:10** Ay 1:19; Hos 12:1; Yud 12; Eze 15:4; Hos 13:15
[g]**17:12** Eze 12:9; 2Fal 24:15; Kum 21:10; 2Nya 36:10; Eze 24:19
[h]**17:13** 2Nya 36:13; 2Fal 24:17; Kut 23:32; Isa 3:2
[i]**17:14** Eze 29:14
[j]**17:15** Yer 52:3; Kum 17:16; Isa 30:2; Za 56:7; Kum 17:16; Yer 34:3; Eze 29:16
[k]**17:16** Yer 52:11; Eze 12:13; Yer 32:5; 2Fal 24:17
[l]**17:17** Yer 37:7; Eze 4:2; Isa 36:6; Mao 4:17; Eze 29:6-7
[m]**17:18** 2Fal 10:15; 1Nya 29:24
[n]**17:19** Yer 7:9; Hos 10:4; Eze 16:59; 21:23
[o]**17:20** Yos 10:16-18; Mhu 9:12; Eze 12:13; 32:3; 20:36; 15:8; Yer 2:35
[p]**17:21** Eze 12:14; 2Fal 25:11; Law 26:33; Zek 2:5-6; 2Fal 25:5

*Hatimaye Israeli Kutukuzwa*

22 [a]" 'Hili ndilo BWANA Mwenyezi
asemalo: Mimi mwenyewe nitachukua
chipukizi kutoka kwenye kilele cha juu
sana cha mwerezi na kukipanda, nitavunja
kitawi kichanga kutoka matawi yake ya
juu kabisa na kukipanda juu ya mlima
mrefu ulioinuka sana. 23 [b]Katika vilele
vya mlima mrefu wa Israeli nitakipanda,
kitatoa matawi na kuzaa matunda na kuwa
mwerezi mzuri sana. Ndege wa kila aina
wataweka viota vyao ndani yake, nao
watapata makazi katika kivuli cha matawi
yake. 24 [c]Miti yote ya kondeni itajua kuwa
Mimi BWANA ninaishusha miti mirefu na
kuikuza miti mifupi kuwa miti mirefu. Mimi
naikausha miti mibichi na kuifanya miti
mikavu istawi.

" 'Mimi BWANA nimesema, nami nitatenda.' "

*Roho Itendayo Dhambi Itakufa*

18 Neno la BWANA likanijia kusema:
2 [d]"Je, ninyi watu mna maana gani
kutumia mithali hii inayohusu nchi ya
Israeli:

" 'Baba wamekula zabibu zenye
chachu,
nayo meno ya watoto yametiwa
ganzi'?

3 [e]"Hakika kama niishivyo, asema BWANA
Mwenyezi, hamtatumia tena mithali hii
katika Israeli. 4 [f]Kwa kuwa kila roho ni mali
yangu, kama vile ilivyo roho ya baba, vivyo
hivyo roho ya mtoto ni mali yangu. Roho
itendayo dhambi ndiyo itakayokufa.

5 "Mtu aweza kuwa ni mwenye haki
atendaye yaliyo haki na sawa.
6 [g]Hakula katika mahali pa ibada za
miungu
kwenye milima
wala hakuziinulia macho sanamu
za nyumba ya Israeli.
Hakumtia unajisi mke wa jirani
yake,
wala hakukutana kimwili na
mwanamke
wakati wa siku zake za hedhi.
7 [h]Hamwonei mtu yeyote,
bali hurudisha kilichowekwa
rehani kwake.
Hanyang'anyi, bali huwapa wenye
njaa chakula chake
na huwapa nguo walio uchi.
8 [i]Hakopeshi kwa riba
wala hajipatii faida ya ziada.
Huuzuia mkono wake usifanye
mabaya,
naye huhukumu kwa haki kati ya
mtu na mtu.
9 [j]Huzifuata amri zangu
na kuzishika sheria zangu kwa
uaminifu.
Huyo mtu ni mwenye haki;
hakika ataishi,
asema BWANA Mwenyezi.

10 [k]"Aweza kuwa ana mwana jeuri,
amwagaye damu au atendaye mojawapo
ya mambo haya 11 [l](ingawa baba yake
hakufanya mojawapo ya haya):

"Hula katika mahali pa ibada za
miungu kwenye milima.
Humtia unajisi mke wa jirani yake.

---

[a]**17:22** Isa 2:2; 53:2; Yer 23:5; 2Fal 19:30; Isa 4:2; Eze 20:40; 40:2; 43:12
[b]**17:23** Dan 4:12; Mt 13:32; Mik 4:1; Yer 31:12; Isa 27:6; 2:2; Za 92:12; Hos 14:5-7
[c]**17:24** Za 96:12; Isa 2:13; Eze 19:12; 21:26; 22:14; Amo 9:11; Za 52:5; Hes 17:8; Dan 5:21; 1Sam 2:7-8; Eze 37:13
[d]**18:2** Isa 3:15; Mao 5:7; Ay 21:19; Yer 31:29
[e]**18:3** Za 49:4
[f]**18:4** Mwa 18:32; Rum 6:23; Ebr 12:9; 2Fal 14:6; Mit 13:21; Kut 17:14; Ay 21:20; Isa 42:5; Eze 33:8
[g]**18:6** Eze 6:2; 22:9; Kum 4:19; Amo 5:26; Ebr 13:4; Eze 6:13; Law 15:24
[h]**18:7** Yak 5:4; Kut 22:26; Kum 24:12; 24:12; 15:11; Lk 3:11; Kut 20:15; Ay 22:7
[i]**18:8** Zek 8:16; Kut 18:21; Kum 23:19-20; Yer 22:3; Kut 22:25; Law 25:35-37
[j]**18:9** Hab 2:4; Law 18:5; Amo 5:4; Law 19:37; Eze 11:12; 20:11
[k]**18:10** Kut 21:12; Eze 22:6
[l]**18:11** Kut 22:22; Ay 24:9; Isa 54:9; 59:6-7; Hab 2:6; Kut 22:17; Eze 16:49

12 [a]Huwaonea maskini na wahitaji.
Hunyang'anyana.
Harudishi kile kilichowekwa rehani kwake.
Huziinulia sanamu macho.
Hufanya mambo ya machukizo.
13 [b]Hukopesha kwa riba na kutafuta faida ya ziada.

Je, mtu wa namna hii ataishi? Hapana, hataishi! Kwa sababu amefanya mambo haya yote ya machukizo, hakika atauawa na damu yake itakuwa juu ya kichwa chake mwenyewe.
14 [c]"Lakini yawezekana mwana huyo ana mwana aonaye dhambi hizi zote anazofanya baba yake, naye ingawa anaziona, yeye hafanyi mabaya kama haya:

15 [d]"Hakula katika mahali pa ibada za miungu
kwenye milima,
wala hainulii macho sanamu
za nyumba ya Israeli.
Hakumtia unajisi
mke wa jirani yake.
16 [e]Hakumwonea mtu yeyote
wala hakutaka rehani kwa ajili ya mkopo.
Hanyang'anyi,
bali huwapa wenye njaa chakula chake
na huwapa nguo walio uchi.
17 [f]Huuzuia mkono wake usitende dhambi,
hakopeshi kwa riba
wala hajipatii faida ya ziada.
Huzishika amri zangu
na kuzifuata sheria zangu.

Hatakufa kwa ajili ya dhambi za baba yake;
hakika ataishi. 18 [g]Lakini baba yake atakufa
kwa ajili ya dhambi yake mwenyewe, kwa sababu alitoza bei isiyo halali kwa nguvu, akamnyang'anya ndugu yake na kufanya yaliyo mabaya miongoni mwa watu wake.
19 [h]"Lakini mnauliza, 'Kwa nini mwana asiadhibiwe kwa uovu wa baba yake?' Kwa vile mwana ametenda yaliyo haki na sawa na amekuwa mwangalifu kuzishika
amri zangu zote, hakika ataishi. 20 [i]Roho
itendayo dhambi ndiyo itakayokufa. Mwana hataadhibiwa kwa ajili ya makosa ya baba yake, wala baba hataadhibiwa kwa ajili ya makosa ya mwanawe. Haki ya mtu mwenye haki itahesabiwa juu yake na uovu wa mtu mwovu utalipizwa juu yake.
21 [j]"Lakini mtu mwovu akiacha dhambi zake zote alizozitenda na kushika amri zangu zote na kufanya lililo haki na sawa, hakika
ataishi, hatakufa. 22 [k]Hakuna kosa lolote
alilotenda litakalokumbukwa juu yake. Kwa ajili ya mambo ya haki aliyoyatenda,
ataishi. 23 [l]Je, mimi ninafurahia kifo cha
mtu mwovu? Asema BWANA Mwenyezi. Je, si mimi ninafurahi wanapogeuka kutoka njia zao mbaya na kuishi?
24 [m]"Lakini kama mtu mwenye haki akiacha haki yake na kutenda dhambi na kufanya mambo ya machukizo ambayo mtu mwovu hufanya, Je, ataishi? Hakuna hata mojawapo ya matendo ya haki aliyotenda litakalokumbukwa. Kwa sababu ya kukosa uaminifu kwake anayo hatia na kwa sababu ya dhambi alizozitenda, atakufa.
25 [n]"Lakini mnasema, 'Njia ya Bwana si ya haki.' Sikia, ee nyumba ya Israeli: Njia yangu siyo iliyo ya haki? Je, si njia zenu

[a]**18:12** Kut 22:22; 22:27; Ay 24:9; Amo 4:1; 2Fal 21:11
[b]**18:13** Kut 22:25; Law 20:9; Hos 12:14; Eze 33:4-5
[c]**18:14** 2Nya 34:21; Mit 23:24
[d]**18:15** Eze 22:9; Za 24:4
[e]**18:16** Kut 22:27; Ay 22:7; Mit 22:9; Za 41:1; Eze 16:49; Isa 7:10
[f]**18:17** Za 1:2
[g]**18:18** Eze 3:18
[h]**18:19** Kut 20:5; Kum 5:9; Yer 15:4; Zek 1:3-6
[i]**18:20** Kum 24:16; Rum 2:9; Isa 3:10; Hes 15:31; 1Fal 8:32; 2Fal 14:6; Eze 7:27; Mt 16:27
[j]**18:21** Eze 13:22; 33:12-19; Yer 18:8; Mwa 26:5
[k]**18:22** Dan 4:27; Mik 7:19; Mit 18:20-24; Isa 43:25
[l]**18:23** Mao 3:33; 2Pet 3:9; 1Tim 2:4; Za 147:11; Ay 37:23; Eze 16:6; Mik 7:18
[m]**18:24** Ay 35:8; 2Pet 2:20-22; Ebr 10:38; Yer 34:6; Eze 15:8; 1Sam 15:11; 2Nya 24:17-20
[n]**18:25** Sef 3:5; Mal 3:1-17; Mwa 18:25; Yer 2:29; Eze 33:17; Mal 2:17

ndizo ambazo si za haki? 26 [a]Kama mtu
mwenye haki akiacha haki yake na kutenda
dhambi, atakufa kwa ajili ya dhambi
yake, kwa sababu ya dhambi alizotenda,
atakufa. 27 [b]Lakini mtu mwovu akigeuka
kutoka maovu aliyoyatenda na kufanya
yaliyo haki na sawa, ataokoa maisha yake.
28 [c]Kwa kuwa anayafikiria na kugeuka
kutoka makosa yake yote aliyoyatenda
na kuyaacha, hakika ataishi, hatakufa.
29 Lakini nyumba ya Israeli inasema, 'Njia
za Bwana si haki.' Je, njia zangu si za haki,
ee nyumba ya Israeli? Je, si njia zenu ndizo
ambazo si za haki?"

30 [d]"Kwa hiyo, ee nyumba ya Israeli,
nitawahukumu, kila mmoja sawasawa
na njia zake, asema BWANA Mwenyezi.
Tubuni! Geukeni kutoka makosa yenu
yote, ndipo dhambi haitakuwa anguko
lenu. 31 [e]Tupilieni mbali makosa yenu yote
mliyoyatenda, nanyi mpate moyo mpya na
roho mpya. Kwa nini mfe, ee nyumba ya
Israeli? 32 [f]Kwa maana sifurahii kifo cha
mtu awaye yote afaye katika uovu, asema
BWANA Mwenyezi. Tubuni basi, mkaishi!

*Maombolezo Kwa Ajili Ya Wakuu Wa Israeli*

19 [g]"Wewe fanya maombolezo kuhusu
wakuu wa Israeli 2 [h]na useme:

" 'Tazama jinsi gani mama yako
alivyokuwa simba jike
miongoni mwa simba!
Alilala katikati ya wana simba
na kulisha watoto wake.
3 [i]Alimlea mmoja wa watoto wake,
naye akawa simba mwenye nguvu.
Akajifunza kurarua mawindo
naye akala watu.
4 [j]Mataifa wakasikia habari zake,
naye akanaswa katika shimo lao.
Wakamwongoza kwa ndoana
mpaka nchi ya Misri.

5 [k]" 'Mama yake alipongoja na kuona
tumaini lake halitimiziki,
nayo matarajio yake yametoweka,
akamchukua mwanawe mwingine
na kumfanya simba mwenye
nguvu.
6 [l]Alizungukazunguka miongoni mwa
simba,
kwa kuwa sasa alikuwa simba
mwenye nguvu.
Akajifunza kurarua mawindo
naye akala watu.
7 [m]Akabomoa ngome zao
na kuiharibu miji yao.
Nchi na wote waliokuwa ndani yake
wakatiwa hofu kwa kunguruma
kwake.
8 [n]Kisha mataifa wakaja dhidi yake
kutoka sehemu zilizomzunguka.
Wakatanda nyavu zao kwa ajili yake,
naye akanaswa katika shimo lao.
9 [o]Kwa kutumia ndoana wakamvutia
kwenye tundu
na kumleta mpaka kwa mfalme wa
Babeli.
Wakamtia gerezani, hivyo
kunguruma kwake
hakukusikika tena
katika milima ya Israeli.

10 [p]" 'Mama yako alikuwa kama
mzabibu
katika shamba lako la mizabibu
uliopandwa kando ya maji,

[a]**18:26** Eze 18:24
[b]**18:27** Isa 1:18; Eze 13:22
[c]**18:28** Eze 18:14; Isa 55:7
[d]**18:30** Yer 35:15; Eze 7:13; Mt 3:2; Hos 12:6; 1Pet 1:17; Isa 27
[e]**18:31** Za 51:10; Isa 1:16-17; Eze 36:26; Efe 4:22; Amu 6:8; Yer 27:13; Eze 11:19
[f]**18:32** 2Nya 7:14; Ay 37:23; Eze 33:11; Ay 22:23; Isa 55:7; Mal 3:7; Eze 16:6
[g]**19:1** Yer 7:29; 2Nya 24:6; Eze 26:17; Yer 9:10, 20; Eze 27:32; 28:12
[h]**19:2** Hes 23:24; Mwa 49:9
[i]**19:3** Eze 19:6; 2Fal 23:31, 32
[j]**19:4** 2Nya 36:4; Mao 4:20; Ay 41:2; 2Fal 23:33-34
[k]**19:5** 2Fal 23:34; Mwa 49:9
[l]**19:6** Yer 22:13; 2Nya 36:9; 2Fal 24:9
[m]**19:7** Eze 29:10; 30:12
[n]**19:8** 2Fal 24:2, 11; Mao 4:20; Eze 12:13; 2Fal 24:11
[o]**19:9** 2Fal 25:7; 24:15; 2Nya 36:6; 2Fal 19:28; Zek 11:3
[p]**19:10** Za 80:8-11; Eze 15:2; Yer 17:8; Mwa 49:22

ukiwa unazaa sana na wenye matawi mengi
kwa sababu ya wingi wa maji.
11 [a]Matawi yake yalikuwa na nguvu,
yaliyofaa kuwa fimbo ya enzi ya mtawala.
Ulikuwa mrefu kupita miti mingine
katikati ya matawi manene;
ulionekana kwa urahisi
kwa ajili ya urefu wake
na wingi wa matawi yake.
12 [b]Lakini uling'olewa kwa hasira kali
na kutupwa chini.
Upepo wa mashariki uliufanya usinyae,
matunda yake yakapukutika,
matawi yake yenye nguvu yakanyauka
na moto ukayateketeza.
13 [c]Sasa umepandwa jangwani
katika nchi kame na ya kiu.
14 [d]Moto ulienea kuanzia katika mmojawapo ya matawi yake makubwa
na kuteketeza matunda yake.
Hakuna tawi lenye nguvu lililobaki juu yake
lifaalo kuwa fimbo ya enzi ya mtawala.'

Hili ndilo ombolezo, na litumike kama ombolezo."

*Israeli Waasi*

20 [e]Katika mwaka wa saba, mwezi wa tano siku ya kumi, baadhi ya wazee wa Israeli wakaja ili kutaka ushauri kwa BWANA, wakaketi mbele yangu.
2 Ndipo neno la BWANA likanijia kusema:
3 [f]"Mwanadamu, sema na wazee wa Israeli uwaambie, 'Hili ndilo BWANA Mwenyezi asemalo: Kwa nini mmekuja? Je, ni kutaka ushauri kwangu? Hakika kama niishivyo, sitawaruhusu mtake ushauri toka kwangu, asema BWANA Mwenyezi.'
4 [g]"Je, utawahukumu? Je, mwanadamu, utawahukumu? Basi uwakabili kwa ajili ya machukizo ya baba zao
5 [h]na uwaambie: 'Hili ndilo BWANA Mwenyezi asemalo: Siku ile nilipochagua Israeli, niliwaapia wazao wa nyumba ya Yakobo kwa mkono ulioinuliwa nami nikajidhihirisha kwao huko Misri. Kwa mkono ulioinuliwa niliwaambia, "Mimi ndimi BWANA, Mungu wenu."
6 [i]Siku ile niliwaapia wao kwamba nitawatoa katika nchi ya Misri na kuwaleta katika nchi niliyowachagulia, nchi itiririkayo maziwa na asali, nchi nzuri kupita zote.
7 [j]Nami nikawaambia, "Kila mmoja wenu aondolee mbali sanamu za chukizo ambazo mmekazia macho, nanyi msijitie unajisi kwa sanamu za Misri. Mimi ndimi BWANA, Mungu wenu."
8 [k]" 'Lakini waliniasi na hawakunisikiliza, hawakuondolea mbali sanamu za machukizo ambazo walikuwa wamezikazia macho, wala kuondolea mbali sanamu za Misri. Ndipo nikasema, nitawamwagia ghadhabu yangu na kutimiza hasira yangu dhidi yao huko Misri.
9 [l]Lakini kwa ajili ya Jina langu nilifanya kile ambacho kingelifanya lisitiwe unajisi machoni mwa mataifa waliyoishi miongoni mwao na ambao machoni pao nilikuwa nimejifunua kwa Waisraeli kwa kuwatoa katika nchi ya Misri.
10 [m]Kwa hiyo nikawaongoza watoke Misri na kuwaleta jangwani.
11 [n]Nikawapa amri zangu na kuwajulisha sheria zangu, kwa kuwa mtu

[a]**19:11** Eze 31:3; Dan 4:11
[b]**19:12** Kum 29:28; Eze 17:10; Hos 13:15; Isa 27:11; Eze 28:17; Mwa 41:6
[c]**19:13** Eze 20:35; Hos 2:14; 2:3
[d]**19:14** Amu 9:15; Eze 20:47; 15:4
[e]**20:1** Eze 8:1; 1:1-2; 21:1; Mwa 25:22
[f]**20:3** Mwa 25:22; Eze 14:3; 1Sam 28:6; Amo 8:12; Mit 15:8; Mt 15:8; Isa 1:15
[g]**20:4** Eze 22:2; 23:36; 16:2
[h]**20:5** Kum 7:6; Law 11:44; Kut 20:2; Kum 4:34; Mwa 14:22; Hes 14:30
[i]**20:6** Kut 3:8; Dan 8:9; Za 48:2; Dan 11:41; Kut 6:8; Kum 29:18
[j]**20:7** Kut 20:2-4; Law 18:3; Eze 6:9; Kum 29:18
[k]**20:8** Yer 11:10; Eze 16:26; Kut 32:7; Kum 9:7; Isa 63:10; Yer 7:26
[l]**20:9** Eze 36:22; 39:7; Kut 32:12; Hes 14:13; Isa 48:11
[m]**20:10** Kut 13:18
[n]**20:11** Kut 20:1-23; Rum 10:5; Neh 9:13; Eze 18:9; Kum 4:7-8; Law 18:5

anayezitii ataishi kwa hizo. 12 [a]Pia niliwapa
Sabato zangu kama ishara kati yangu
nao, ili wapate kujua kuwa Mimi BWANA
niliwafanya kuwa watakatifu.
13 [b]“ ‘Lakini watu wa Israeli waliniasi
Mimi jangwani. Hawakufuata amri zangu,
bali walikataa sheria zangu, ingawa mtu
yule anayezitii ataishi kwa hizo sheria, nao
walizinajisi Sabato zangu kabisa. Hivyo
nilisema ningemwaga ghadhabu yangu
juu yao na kuwaangamiza huko jangwani.
14 [c]Lakini kwa ajili ya Jina langu nikafanya
kile ambacho kitalifanya Jina langu lisitiwe
unajisi machoni mwa mataifa ambao mbele
yao nilikuwa nimewatoa Waisraeli. 15 [d]Tena
kwa mkono ulioinuliwa nikawaapia huko
jangwani kwamba nisingewaingiza katika
nchi niliyokuwa nimewapa, yaani, nchi
itiririkayo maziwa na asali, nchi nzuri
kuliko zote, 16 [e]kwa sababu walikataa
sheria zangu na hawakufuata amri zangu
na wakazinajisi Sabato zangu. Kwa kuwa
mioyo yao iliandama sanamu zao. 17 [f]Lakini
niliwahurumia wala sikuwaangamiza
wala hakuwafuta kabisa jangwani.
18 [g]Niliwaambia watoto wao kule jangwani,
“Msifuate amri za baba zenu wala kushika
sheria zao au kujinajisi kwa sanamu zao.
19 [h]Mimi ndimi BWANA, Mungu wenu,
fuateni amri zangu tena kuweni waangalifu
kushika sheria zangu. 20 [i]Zitakaseni Sabato
zangu ili ziwe ishara kati yangu nanyi.
Ndipo mtakapojua kuwa Mimi ndimi
BWANA, Mungu wenu.”
21 [j]“ ‘Lakini watoto hao wakaniasi:
Hawakufuata amri zangu, wala hawakuwa
waangalifu kushika sheria zangu, ingawa
mtu anayezitii anaishi kwa hizo sheria,
nao wakazinajisi Sabato zangu. Hivyo
nikasema ningemwaga ghadhabu yangu
juu yao na kutimiza hasira yangu dhidi
yao huko jangwani. 22 [k]Lakini nikauzuia
mkono wangu na kwa ajili ya Jina langu
nikafanya kile ambacho kingelifanya Jina
langu lisitiwe unajisi machoni mwa mataifa
ambao mbele yao nilikuwa nimewatoa
Waisraeli. 23 [l]Tena kwa mkono ulioinuliwa
nikawaapia huko jangwani kwamba
ningewatawanya miongoni mwa mataifa
na kuwatawanya katika nchi mbalimbali,
24 [m]kwa sababu hawakutii sheria zangu
lakini walikuwa wamekataa amri zangu
na kuzinajisi Sabato zangu, nayo macho
yao yakatamani sanamu za baba zao. 25 [n]Pia
niliwaacha wafuate amri ambazo hazikuwa
nzuri na sheria ambazo mtu hawezi kuishi
kwa hizo sheria. 26 [o]Nikawaacha wanajisiwe
kwa matoleo yao, kuwatoa wazaliwa wao
wa kwanza kafara kwa sanamu, yaani, kule
kuwapitisha wazaliwa wao wa kwanza
kwenye moto, nipate kuwajaza na hofu ili
wajue kwamba Mimi ndimi BWANA.’
27 [p]“Kwa hiyo, mwanadamu, sema na
watu wa Israeli na uwaambie, ‘Hili ndilo
BWANA Mwenyezi asemalo: Katika hili pia,
baba zenu walinikufuru kwa kuniacha mimi:
28 [q]Nilipowaleta katika nchi ile ambayo
nilikuwa nimeapa kuwapa na kuona kilima
chochote kirefu au mti wowote wenye
majani mengi, huko walitoa dhabihu zao,
wakatoa sadaka ambazo zilichochea hasira
yangu, wakafukiza uvumba wenye harufu
nzuri na kumimina sadaka zao za kinywaji.
29 Ndipo nikawaambia: Ni nini maana yake
hapa mahali pa juu pa kuabudia miungu

[a]**20:12** Kut 31:13; Kum 5:12; Kut 20:10; Yer 17:22; Law 20:8
[b]**20:13** Za 78:40; Kum 9:8; Law 26:15; Hes 14:29; Za 95:8-10; Isa 56:6; Kut 32:10
[c]**20:14** Eze 36:23; Isa 48:11
[d]**20:15** Hes 14:22-23, 28; Ebr 3:11; Kum 1:34; Za 106:26; 95:11
[e]**20:16** Hes 16:39; Amo 5:26; Mdo 7:42-43; Yer 1:8; Amo 2:4; Hes 15:39
[f]**20:17** Za 78:38
[g]**20:18** 2Nya 30:7; Za 106; 39
[h]**20:19** Kut 20:2; Kum 11:1; 5:32-33
[i]**20:20** Yer 17:22; Kut 20:10; 31:13
[j]**20:21** Yer 7:26; Hes 25:3; Eze 7:8
[k]**20:22** Za 78:38
[l]**20:23** Law 26:33; Kum 28:64; Za 106:27; Yer 15:4
[m]**20:24** Eze 2:3; 6:9; 18:6; Amo 2:4
[n]**20:25** Za 81:12; Rum 1:24-28; 2The 2:11; Isa 66:4
[o]**20:26** Law 20:2-5; 2Fal 17:17; Eze 16:20-21; Law 18:21
[p]**20:27** Hes 15:30; Rum 1:23; 2:24; Eze 18:24; Za 78:57
[q]**20:28** Neh 9:23; Za 78:55-58; Yer 19:13; Eze 6:13; Yer 2:7; 3:6

mnapopaendea?’ ” (Basi jina la mahali pale
panaitwa Bama[a] hata hivi leo.)

*Hukumu Na Kurudishwa*

30 [b]“Kwa hiyo iambie nyumba ya Israeli:
‘Hili ndilo Bwana Mwenyezi asemalo:
Je, mtajinajisi kama vile baba zenu
walivyofanya na kutamani vinyago vyao
vya machukizo? 31 [c]Mnapotoa matoleo
yenu, yaani, wana wenu kafara katika moto,
mnaendelea kujinajisi na sanamu zenu zote
hadi siku hii ya leo. Je, niulizwe neno na
ninyi, ee nyumba ya Israeli? Hakika kama
niishivyo, asema Bwana Mwenyezi, mimi
sitaulizwa neno na ninyi.
32 [d]“ ‘Lile lililoko mioyoni mwenu kamwe
halitatokea, mnaposema, “Tunataka tuwe
kama mataifa mengine, kama watu wengine
wa dunia, wanaotumikia miti na mawe.”
33 [e]Hakika kama niishivyo asema Bwana
Mwenyezi, nitatawala juu yenu kwa mkono
wa nguvu na kwa mkono ulionyooshwa na
kwa ghadhabu iliyomwagwa. 34 [f]Nitawatoa
toka katika mataifa na kuwakusanya
kutoka nchi mlikotawanywa, kwa mkono
wa nguvu na kwa mkono ulionyooshwa
na kwa ghadhabu iliyomwagwa.
35 [g]Nitawaleta katika jangwa la mataifa
na huko nitatekeleza hukumu juu yenu
uso kwa uso. 36 [h]Kama nilivyowahukumu
baba zenu katika jangwa la nchi ya Misri,
ndivyo nitakavyowahukumu ninyi, asema
Bwana Mwenyezi. 37 [i]Nitawafanya mpite
chini ya fimbo yangu, nami nitawaleta
katika mkataba wa Agano. 38 [j]Nitawaondoa
miongoni mwenu wale wanaohalifu na wale
wanaoasi dhidi yangu. Ingawa nitawatoa
katika nchi wanazoishi, hawataingia katika
nchi ya Israeli. Ndipo mtakapojua kuwa
Mimi ndimi Bwana.
39 [k]“ ‘Kwa habari zenu ninyi, ee nyumba
ya Israeli, hili ndilo Bwana Mwenyezi
asemalo: Nendeni mkatumikie sanamu zenu,
kila mmoja wenu! Lakini baadaye hakika
mtanisikiliza mimi nanyi hamtalinajisi tena
Jina langu takatifu, kwa matoleo yenu na
sanamu zenu. 40 [l]Kwa kuwa katika mlima
wangu mtakatifu, mlima mrefu wa Israeli,
asema Bwana Mwenyezi, hapo katika nchi
nyumba yote ya Israeli itanitumikia mimi,
nami huko nitawakubali. Huko nitataka
sadaka zenu na matoleo ya malimbuko
yenu, pamoja na dhabihu zenu takatifu
zote. 41 [m]Nitawakubali ninyi kama uvumba
wenye harufu nzuri wakati nitakapowatoa
katika mataifa na kuwakusanya kutoka
nchi mlipokuwa mmetawanyika, nami
nitajionyesha kuwa mtakatifu miongoni
mwenu na machoni mwa mataifa. 42 [n]Ndipo
mtakapojua kuwa Mimi ndimi Bwana,
nitakapowaleta katika nchi ya Israeli, nchi
niliyokuwa nimeapa kwa mkono ulioinuliwa
kuwapa baba zenu. 43 [o]Hapo ndipo
nitakapokumbuka mwenendo wenu na
matendo yenu yote ambayo kwayo mlijitia
unajisi, nanyi mtajichukia wenyewe kwa
ajili ya maovu yote mliyokuwa mmetenda.
44 [p]Nanyi mtajua kuwa mimi ndimi Bwana,
nitakaposhughulika nanyi kwa ajili ya Jina
langu na wala si sawasawa na njia zenu
mbaya na matendo yenu maovu, ee nyumba
ya Israeli, asema Bwana Mwenyezi.’ ”

[a]29 Bama maana yake ni mahali pa juu pa kuabudia miungu.
[b]**20:30** Amu 2:16-19; Yer 16:12
[c]**20:31** Mit 1:27-28; Eze 16:20; Amo 8:12; Zek 7:13; Za 106:37-39; Yer 7:31
[d]**20:32** Eze 11:5
[e]**20:33** Yer 21:5; Eze 25:16; 16:27
[f]**20:34** 2Kor 6:17; Yer 44:6; Mao 2:4; Kum 30:4; Isa 27:12-13; 31:3
[g]**20:35** 1Sam 12:7; Ay 22:4; Eze 19:13; Yer 2:35
[h]**20:36** Hes 14:28-30; 1Kor 10:5-10; Hes 11:1-35
[i]**20:37** Law 27:32; Yer 33:13; Eze 16:62
[j]**20:38** Eze 34:17-22; Amo 9:9-10; Hos 2:14; Ebr 4:3; Za 95:11; Eze 13:9; Zek 13:8-9
[k]**20:39** Yer 44:25; Isa 1:13; Amo 4:4; Mit 21:27; Kut 20:7; Eze 13:19; 43:7
[l]**20:40** Isa 60:7; 56:7; Mal 3:4; Zek 8:20; Rum 12:1; Eze 17:22; 34:14
[m]**20:41** Eze 28:25; 36:23; Isa 5:16; 2Kor 6:17; 2:14; Kum 30:4
[n]**20:42** Eze 38:23; Yer 23:8; Eze 36:24; Yer 30:3; Eze 34:13; 34:27
[o]**20:43** Eze 16:61; Law 26:39; Eze 6:9; Hos 5:15
[p]**20:44** Za 109:21; Isa 43:25; Eze 24:24; 36:32

*Unabii Dhidi Ya Kusini*

45 Neno la BWANA likanijia kusema:
46 [a]"Mwanadamu, uelekeze uso wako
upande wa kusini, hubiri juu ya upande
wa kusini na utoe unabii juu ya msitu wa
Negebu. 47 [b]Waambie watu wa Negebu:
'Sikieni neno la BWANA. Hili ndilo BWANA
Mwenyezi asemalo: Ninakaribia kukutia
moto, nao utateketeza miti yako yote,
mibichi na iliyokauka. Miali ya moto
haitaweza kuzimwa na kila uso kutoka
kusini mpaka kaskazini utakaushwa kwa
moto huo. 48 [c]Kila mmoja ataona kuwa mimi
BWANA ndiye niliyeuwasha huo moto, nao
hautazimwa.' "

49 [d]Ndipo niliposema, "Aa, BWANA
Mwenyezi! Wao hunisema, 'Huyu si
huzungumza mafumbo tu?' "

*Babeli, Upanga Wa Mungu Wa Hukumu*

21 [e]Neno la BWANA likanijia kusema:
2 [f]"Mwanadamu, uelekeze uso wako
juu ya Yerusalemu na uhubiri dhidi ya
mahali patakatifu. Tabiri dhidi ya nchi
ya Israeli 3 [g]uiambie: 'Hili ndilo BWANA
asemalo: Mimi niko kinyume nawe.
Nitautoa upanga wangu kwenye ala yake
na kumkatilia mbali mwenye haki na
mwovu. 4 [h]Kwa sababu nitamkatilia mbali
mwenye haki na mwovu, upanga wangu
utakuwa wazi dhidi ya kila mmoja kuanzia
kusini mpaka kaskazini. 5 [i]Ndipo watu wote
watajua ya kuwa Mimi BWANA nimeutoa
upanga wangu kwenye ala yake, nao
hautarudi humo tena.'

6 [j]"Kwa hiyo lia kwa uchungu,
mwanadamu! Lia kwa uchungu mbele yao
kwa moyo uliopondeka na kwa huzuni
nyingi. 7 [k]Nao watakapokuuliza, 'Kwa nini
unalia kwa uchungu?' Utasema hivi, 'Kwa
sababu ya habari zinazokuja. Kila moyo
utayeyuka na kila mkono utalegea, kila roho
itazimia na kila goti litalegea kama maji.'
Habari hizo zinakuja! Hakika zitatokea,
asema BWANA Mwenyezi."

8 Neno la BWANA likanijia, kusema:
9 [l]"Mwanadamu, tabiri na useme, 'Hili ndilo
Bwana asemalo:

" 'Upanga, upanga,
ulionolewa na kusuguliwa:
10 [m]umenolewa kwa ajili ya mauaji,
umesuguliwa ili ung'ae
kama umeme wa radi!

" 'Je, tuifurahie fimbo ya utawala ya
mwanangu Yuda? Upanga unaidharau kila
fimbo ya namna hiyo.

11 [n]" 'Upanga umewekwa tayari ili
kusuguliwa,
ili upate kushikwa mkononi,
umenolewa na kusuguliwa,
umewekwa tayari kwa mkono wa
muuaji.
12 [o]Piga kelele na uomboleze, ee
mwanadamu,
kwa kuwa upanga u dhidi ya watu
wangu;
u dhidi ya wakuu wote wa Israeli.
Wametolewa wauawe kwa upanga
pamoja na watu wangu.
Kwa hiyo pigapiga kifua chako.

13 [p]" 'Kwa maana upanga huu umejaribiwa
na kuhakikishwa, itakuwaje basi fimbo
ya ufalme ya Yuda inayoudharau
kama haitakuwepo tena, bali itakuwa
imeondolewa kabisa? asema BWANA
Mwenyezi.'

---

[a]**20:46** Eze 21:2; Amo 7:16; Isa 30:6; Yer 13:17-19
[b]**20:47** Yer 21:14; Isa 13:8; Eze 21:4; 2Fal 19:23; Isa 9:18-19; Eze 19:14
[c]**20:48** Yer 7:20; Eze 21:5, 32; 23:25
[d]**20:49** Amu 14:12; Yn 16:24-25; Eze 4:14; Za 78:2; Eze 12:9; Mt 13:13
[e]**21:1** Eze 20:1
[f]**21:2** Yer 11:12; Eze 20:46; Amo 7:16; Eze 9:6; 13:17
[g]**21:3** Yer 21:13; 47:6-7; Ay 9:22; Isa 27:1; Eze 14:21
[h]**21:4** Eze 20:47; Law 26:25; Yer 25:27
[i]**21:5** Eze 20:47-48; Isa 45:23; 34:5
[j]**21:6** Isa 22:4; Yer 30:6; Eze 9:4
[k]**21:7** Yer 47:3; Eze 7:17; Ay 23:2; Yos 7:5; Eze 22:14; Za 6:2; Ay 11:16
[l]**21:9** Kum 32:41
[m]**21:10** Za 105:5-6; Isa 34:5-6; Kum 32:41
[n]**21:11** Yer 46:4
[o]**21:12** Yer 31:19
[p]**21:13** Ay 9:23; 2Kor 8:2

14 [a]"Hivyo basi, mwanadamu, tabiri
na ukapige makofi.
Upanga wako na upige mara mbili,
naam, hata mara tatu.
Ni upanga wa kuchinja,
upanga wa mauaji makuu,
ukiwashambulia kutoka kila
upande.
15 [b]Ili mioyo ipate kuyeyuka
na wanaouawa wawe wengi,
nimeweka upanga wa kuchinja
kwenye malango yao yote.
Lo! Umetengenezwa
umetemete kama umeme wa radi,
umeshikwa kwa ajili ya kuua.
16 [c]Ee upanga, kata upande wa kuume,
kisha upande wa kushoto,
mahali popote makali yako
yatakapoelekezwa.
17 [d]Mimi nami nitapiga makofi,
nayo ghadhabu yangu itapungua.
Mimi BWANA nimesema."

18 Neno la BWANA likanijia kusema:
19 [e]"Mwanadamu, weka alama njia mbili
ambazo upanga wa mfalme wa Babeli
utapitia, njia hizo zikianzia katika nchi
hiyo hiyo. Weka kibao pale ambapo njia
zinagawanyika kuelekea mjini. 20 [f]Weka
alama njia moja kwa ajili ya upanga upate
kuja dhidi ya Raba ya Waamoni na nyingine
upate kuja dhidi ya Yuda na Yerusalemu
iliyozungushiwa ngome. 21 [g]Kwa kuwa
mfalme wa Babeli sasa amesimama katika
njia panda, katika makutano ya njia mbili,
akipiga ramli: anapiga kura kwa kutumia
mishale, anataka shauri kwa sanamu
zake, anachunguza maini ya wanyama.
22 [h]Upande wake wa kuume inakuja kura
ya Yerusalemu, ambapo ataweka vyombo
vya kuvunjia boma, ili kuamrisha mauaji,
kupiga ukelele wa vita, kuweka vyombo
vya kuvunjia boma kwenye malango,
kuweka jeshi kuzunguka na kufanya
uzingiraji. 23 [i]Itakuwa kama kupiga
ramli kwa uongo kwa wale watu ambao
wameapa kumtii yeye. Lakini mfalme wa
Babeli atawakumbusha juu ya uovu wao
na kuwachukua mateka.

24 "Kwa hiyo hili ndilo BWANA
Mwenyezi asemalo: 'Kwa sababu enyi
watu mmekumbusha uovu wenu kwa
kuasi waziwazi, mkidhihirisha dhambi
zenu katika yale yote mfanyayo, kwa
kuwa mmefanya jambo hili, mtachukuliwa
mateka.

25 [j]" 'Ee mtawala kafiri na mwovu wa
Israeli, ambaye siku yako imewadia,
ambaye wakati wako wa adhabu umefikia
kilele chake, 26 [k]hili ndilo BWANA
Mwenyezi asemalo: Vua kilemba, ondoa
taji. Kwa kuwa mambo hayatakuwa kama
yalivyokuwa. Aliye mnyonge atakwezwa
na aliyekwezwa atashushwa. 27 [l]Mahame!
Mahame! Nitaufanya mji kuwa mahame!
Hautajengwa upya mpaka aje yule ambaye
ndiye mwenye haki nao; yeye ndiye
nitakayempa.'

28 [m]"Nawe, mwanadamu, tabiri na useme,
'Hili ndilo BWANA Mwenyezi asemalo
kuhusu Waamoni na matukano yao.

" 'Upanga, upanga,
umefutwa kwa ajili ya kuua,
umesuguliwa ili kuangamiza
na unametameta kama umeme wa
radi!
29 [n]Wakati wakitoa maono ya uongo
kwa ajili yako,
wanapobashiri uongo kwa ajili
yako,
wanakuweka wewe kwenye shingo
za watu wapotovu,
wale walio waovu,

[a]**21:14** Hes 24:10; Eze 6:11; 30:24; 8:12
[b]**21:15** 2Sam 17:10; Za 22:14
[c]**21:16** Eze 14:17
[d]**21:17** Eze 22:13; 5:13; 14:17; 16:42
[e]**21:19** Eze 14:21; 32:11; Yer 31:21
[f]**21:20** Yer 49:2; Amo 1:14; Kum 3:11
[g]**21:21** Mit 16:33; Hes 20:7; 23:23; Zek 10:2
[h]**21:22** 2Fal 25:1; Eze 4:2; Yer 51:14; 4:16; 32:24; Eze 26:9
[i]**21:23** Hes 5:15; Eze 17:19
[j]**21:25** Eze 35:5; Mwa 13:13; Eze 22:4
[k]**21:26** Isa 28:5; Yer 13:18; Isa 40:4; Mt 23:12; Za 75:7
[l]**21:27** Mwa 49:10; Za 2:6; Hag 2:21-22; Yer 23:5-6; Eze 37:24
[m]**21:28** Mwa 19:38; Sef 3:8; Yer 12:12
[n]**21:29** Eze 22:28; 35:5; Yer 27:9

wale ambao siku yao imewadia,
wakati wa adhabu yao ya mwisho.
30 [a]Urudishe upanga kwenye ala yake!
Katika mahali ulipoumbiwa,
katika nchi ya baba zako,
huko nitakuhukumu.
31 [b]Nitamwaga ghadhabu yangu juu yako
na kupuliza moto wa hasira yangu dhidi yako;
nitakutia mikononi mwa watu wakatili,
watu stadi katika kuangamiza.
32 [c]Mtakuwa kuni za kuwashia moto,
damu yenu itamwagwa katika nchi yenu,
wala hamtakumbukwa tena;
kwa maana Mimi BWANA nimesema.' "

### *Dhambi Za Yerusalemu*

22 [d]Neno la BWANA likanijia kusema:
2 [e]"Mwanadamu, je, wewe
utauhukumu? Je, utauhukumu huu mji
umwagao damu? Basi uujulishe juu
ya matendo yake yote ya machukizo
3 [f]uuambie: 'Hili ndilo BWANA Mwenyezi
asemalo: Ee mji ule ujileteao maangamizi
wenyewe kwa kumwaga damu ndani yake
na kujinajisi wenyewe kwa kutengeneza
sanamu, 4 [g]umekuwa na hatia kwa sababu
ya damu uliyomwaga na umetiwa unajisi
kwa sanamu ulizotengeneza. Umejiletea
mwisho wa siku zako na mwisho wa miaka
yako umewadia. Kwa hiyo nitakufanya kitu
cha kudharauliwa kwa mataifa na kitu cha
mzaha kwa nchi zote. 5 [h]Wale walio karibu
na wale walio mbali watakudhihaki, Ewe
mji wenye sifa mbaya, uliyejaa ghasia.
6 [i]" 'Ona jinsi kila mkuu wa Israeli
aliyeko ndani yako anavyotumia nguvu
zake kumwaga damu. 7 [j]Ndani yako
wamewadharau baba na mama, ndani
yako wamewatendea wageni udhalimu na
kuwaonea yatima na wajane. 8 [k]Mmedharau
vitu vyangu vitakatifu na kuzinajisi
Sabato zangu. 9 [l]Ndani yako wako watu
wasingiziaji, watu walio tayari kumwaga
damu, ndani yako wako wale wanaokula
vyakula vilivyotolewa mahali pa ibada
za miungu kwenye milima, na kutenda
matendo ya uasherati. 10 [m]Ndani yako
wako wale wanaovunjia heshima vitanda
vya baba zao, ndani yako wamo wale
wanaowatendea wanawake jeuri wakiwa
katika hedhi, wakati wakiwa si safi. 11 [n]Ndani
yako mtu hufanya mambo ya machukizo
na mke wa jirani yake, mwingine kwa
aibu kubwa hukutana kimwili na mke wa
mwanawe, mwingine humtenda jeuri dada
yake, binti wa baba yake hasa. 12 [o]Ndani
yako watu hupokea rushwa ili kumwaga
damu, mnapokea riba na faida ya ziada na
kupata faida isiyokuwa halali kutoka kwa
jirani ili kupata faida kubwa kupita kiasi.
Nawe umenisahau mimi, asema BWANA
Mwenyezi.
13 [p]" 'Hakika nitapiga makofi kwa ajili ya
faida isiyo halali uliyojipatia na kwa damu
uliyoimwaga ndani yako. 14 [q]Je, ujasiri
wako utadumu au mikono yako itakuwa
na nguvu siku hiyo nitakapokushughulikia?
Mimi BWANA nimesema na nitalifanya.

[a]**21:30** Yer 47:6; Eze 16:3
[b]**21:31** Za 79:6; Eze 22:20-21; Yer 51:20-23; Za 18:15; Isa 11:4; Eze 16:39
[c]**21:32** Eze 20:47-48; 25:10; Mal 4:1
[d]**22:1** Hab 2:12; Hos 4:2; Eze 16:2; 23:36; 24:6
[e]**22:2** Eze 24:6, 9; Hos 4:2; Nah 3:1; Hab 2:12; Eze 16:2; 23:36
[f]**22:3** Eze 23:45; 24:2; Mik 6:16
[g]**22:4** 2Fal 21:16; Eze 5:14; 21:25; Za 44:13-14; Dan 9:16; Za 137:3
[h]**22:5** Isa 22:2
[i]**22:6** Isa 1:23; Eze 11:6; 18:10; 33:25
[j]**22:7** Kum 27:16; Mik 7:6; Kut 22:21-22; Kum 5:16; Kut 23:9
[k]**22:8** Kut 20:8; Law 19:30; Eze 23:38-39
[l]**22:9** Law 19:16; Eze 18:11; Hos 4:10-14; Isa 59:3; Eze 23:29
[m]**22:10** Law 12:2; 18:8; 1Kor 5:1
[n]**22:11** Mwa 11:31; Law 18:15; 18:9; 2Sam 13:14; Yer 5:8; Eze 18:9
[o]**22:12** Kut 18:21; Amo 5:12; Law 19:13; Kum 16:19; Za 26:10; Isa 5:23; 17:10
[p]**22:13** Eze 21:17; Hes 24:10; Isa 33:15; Eze 6:11
[q]**22:14** Eze 17:24; 21:7; 24:14; 1Kor 10:22; Za 76:7; Yoe 2:11

15 [a]Nitakutawanya miongoni mwa mataifa
na kukutapanya katika nchi mbalimbali
nami nitakomesha unajisi wako. 16 [b]Ukiisha
kunajisika mbele ya mataifa, utajua kuwa
Mimi ndimi Bwana.' "

17 Ndipo neno la Bwana likanijia kusema:
18 [c]"Mwanadamu, nyumba ya Israeli
imekuwa kwangu takataka ya chuma, wote
kwangu wamekuwa shaba, bati, chuma
na risasi iliyoachwa kalibuni. Wao ni taka
ya madini ya fedha tu. 19 [d]Kwa hiyo hili
ndilo Bwana Mwenyezi asemalo: 'Kwa
kuwa wote mmekuwa takataka ya chuma,
nitawakusanya Yerusalemu. 20 [e]Kama vile
watu wakusanyavyo fedha, shaba, chuma,
risasi na bati kalibuni ili kuyeyusha kwa
moto mkali, ndivyo nitakavyowakusanya
katika hasira yangu na ghadhabu yangu
kuwaweka ndani ya mji na kuwayeyusha.
21 [f]Nitawakusanya na kupuliza juu yenu
moto wa hasira yangu na ghadhabu yangu
nanyi mtayeyushwa ndani ya huo mji.
22 [g]Kama fedha iyeyukavyo kalibuni, ndivyo
mtakavyoyeyuka ndani ya huo mji, nanyi
mtajua kuwa Mimi Bwana nimemwaga
ghadhabu yangu juu yenu.' "

23 Neno la Bwana likanijia tena kusema:
24 [h]"Mwanadamu, iambie nchi, 'Wewe
ni nchi ambayo haijapata mvua wala
manyunyu katika siku ya ghadhabu.'
25 [i]Kuna hila mbaya ya wakuu ndani yake
kama simba angurumaye akirarua mawindo
yake, wanakula watu, wanachukua hazina
na vitu vya thamani na kuongeza idadi ya
wajane ndani yake. 26 [j]Makuhani wake
wameihalifu sheria yangu na kunajisi vitu
vyangu vitakatifu, hawatofautishi kati
ya vitu vitakatifu na vitu vya kawaida.
Wanafundisha kuwa hakuna tofauti kati
ya vitu vilivyo najisi na visivyo najisi, nao
wanafumba macho yao katika kutunza
Sabato zangu, hivyo katikati yao nimetiwa
unajisi. 27 [k]Maafisa wake walioko ndani yake
ni kama mbwa mwitu wararuao mawindo
yao, wanamwaga damu na kuua watu
ili kupata faida ya udhalimu. 28 [l]Manabii
wake wanapaka chokaa matendo haya kwa
maono ya uongo na utabiri wa udanganyifu.
Wanasema, 'Hili ndilo Bwana Mwenyezi
asemalo,' wakati Bwana hajasema.
29 [m]Watu wa nchi wanatoza kwa nguvu na
kufanya unyang'anyi, wanawatenda jeuri
maskini na wahitaji na kuwaonea wageni,
wakiwanyima haki.

30 [n]"Nami nikatafuta mtu miongoni mwao,
ambaye angejenga ukuta na kusimama
mbele zangu mahali palipobomoka kwa ajili
ya watu wa nchi ili nisije nikaiangamiza,
lakini sikumwona mtu yeyote. 31 [o]Hivyo
nitaimwaga ghadhabu yangu juu yao na
kuwateketeza kwa moto wa hasira yangu,
nikiyaleta juu ya vichwa vyao yale yote
waliyotenda, asema Bwana Mwenyezi."

### *Dada Wawili Makahaba*

23 Neno la Bwana likanijia kusema:
2 [p]"Mwanadamu, walikuwepo
wanawake wawili, binti wa mama
mmoja. 3 [q]Wakawa makahaba huko Misri,
wakajitia kwenye ukahaba tangu ujana
wao. Katika nchi ile vifua vyao vya ubikira
vikakumbatiwa huko na wakapoteza
ubikira wao. 4 [r]Mkubwa aliitwa Ohola na
mdogo wake Oholiba. Walikuwa wangu nao

---

[a]**22:15** Kum 4:27; Zek 7:14; Eze 16:41; 23:27; Law 26:33
[b]**22:16** Za 9:16; Eze 6:7
[c]**22:18** Za 119:119; Isa 1:22; Yer 6:28-30; Isa 48:10
[d]**22:19** Za 119:119
[e]**22:20** Hos 8:10; Mal 3:2
[f]**22:21** Isa 40:7; Za 68:2; Eze 21:31
[g]**22:22** Isa 1:25; 64:7; Eze 20:8; 7:8
[h]**22:24** Eze 24:13
[i]**22:25** Hos 9:6; Yer 11:9; 15:8; 18:21; 6:13; Mdo 20:29
[j]**22:26** Hos 9:7-8; Sef 3:4; 1Sam 2:29; Eze 44:23; 42:20; Law 10:10; Hag 2:11-14; Mal 2:7-8; Law 20:25
[k]**22:27** Mwa 37:24; Yer 12:2; 26:10; Mt 7:15; Eze 34:2-3; Isa 1:23
[l]**22:28** Eze 13:6-10; Mao 2:14; 4:13; Eze 21:29; 13:2-7
[m]**22:29** Yer 5:26; Kut 22:21; 23:9; Isa 5:7; Za 106:23
[n]**22:30** Eze 13:5; Za 106:23; Isa 64:7
[o]**22:31** Eze 16:43; 9:10; Rum 2:8; Kut 32:10; Isa 30:27; Mao 4:11; Eze 7:8-9
[p]**23:2** Eze 16:45-46; Yer 3:7
[q]**23:3** Yos 24:14; Law 17:7; Isa 1:21; Za 25:7; Eze 16:15
[r]**23:4** Eze 16:8, 20; 16:46

wakazaa wavulana na msichana. Ohola ni
Samaria, Oholiba ni Yerusalemu.
5 [a]“Ohola akajitia kwenye ukahaba
alipokuwa bado ni wangu, akatamani
sana wapenzi wake, mashujaa Waashuru,
6 waliovaa nguo za buluu, watawala na
majemadari, wote walikuwa wanaume
vijana wa kuvutia, wapandao farasi.
7 [b]Akafanya ukahaba na wasomi wote wa
Ashuru, na kujinajisi kwa sanamu zote za
kila mwanaume aliyemtamani. 8 [c]Hakuacha
ukahaba wake aliouanza huko Misri, wakati
ambapo tangu ujana wake wanaume
walilala naye, wakikumbatia kifua cha
ubikira wake na kumwaga tamaa zao juu
yake.
9 [d]“Kwa hiyo nilimtia mikononi mwa
wapenzi wake, Waashuru, kwa kuwa ndio
aliowatamani. 10 [e]Wakamvua nguo zake
wakamwacha uchi, wakawachukua wanawe
na binti zake, naye wakamuua kwa upanga.
Akawa kitu cha kudharauliwa miongoni
mwa wanawake na adhabu ikatolewa dhidi
yake.
11 [f]“Oholiba dada yake aliliona jambo
hili, lakini kwa tamaa zake na ukahaba
wake, akaharibu tabia zake kuliko Ohola
dada yake. 12 [g]Yeye naye aliwatamani
Waashuru, watawala na majemadari,
mashujaa waliovalia sare, wapandao
farasi, wanaume vijana wote waliovutia.
13 [h]Nikaona kuwa yeye pia alijinajisi, wote
wawili wakaelekea njia moja.
14 [i]“Lakini yeye akazidisha ukahaba
wake. Akaona wanaume waliochorwa
ukutani, picha za Wakaldayo[j] waliovalia
nguo nyekundu, 15 [k]wakiwa na mikanda
viunoni mwao na vilemba vichwani
mwao, wote walifanana na maafisa wa
Babeli wapandao magari ya vita, wenyeji
wa Ukaldayo.[l] 16 [m]Mara tu alipowaona,
aliwatamani, akatuma wajumbe kwao huko
Ukaldayo. 17 [n]Ndipo hao Wababeli wakaja
kwake kwenye kitanda cha mapenzi,
nao katika tamaa zao wakamtia unajisi.
Baada ya kutiwa unajisi, akawaacha
kwa kuwachukia. 18 [o]Alipofanya ukahaba
wake waziwazi na kuonyesha hadharani
uchi wake, nilimwacha kwa kumchukia,
kama vile nilivyokuwa nimemwacha dada
yake. 19 [p]Lakini akazidisha zaidi ukahaba
wake alipozikumbuka siku zake za ujana,
alipokuwa kahaba huko Misri. 20 [q]Huko
aliwatamani wapenzi wake, ambao viungo
vyao vya uzazi ni kama vya punda, na kile
kiwatokacho ni kama kiwatokacho farasi.
21 [r]Hivyo ulitamani uasherati wa ujana
wako wakati ulipokuwa Misri, kifua chako
kilipokumbatiwa, na walipokutomasa kwa
sababu ya matiti yako machanga.
22 [s]“Kwa hiyo, Oholiba, hili ndilo BWANA
Mwenyezi asemalo: Nitawachochea
wapenzi wako wawe kinyume na wewe,
wale uliowaacha kwa kuchukia, nitawaleta
dhidi yako kutoka kila upande: 23 [t]Wababeli
na Wakaldayo wote, watu kutoka Pekodi, na
Shoa na Koa, wakiwa pamoja na Waashuru
wote, vijana wazuri, wote wakiwa watawala
na majemadari, maafisa wa magari ya vita
na watu wa vyeo vya juu, wote wakiwa
wamepanda farasi. 24 [u]Watakuja dhidi
yako wakiwa na silaha, magari ya vita,
magari ya kukokota, pamoja na umati
mkubwa wa watu. Watakuzingira pande
zote kwa ngao na vigao na kofia za chuma.
Nitakutia mikononi mwao ili wakuadhibu,

[a]**23:5** 2Fal 16:7; 15:19; Hos 5:13; 8:9
[b]**23:7** Isa 57:8; Hos 6:10; 5:3
[c]**23:8** Kut 32:4; Eze 16:15
[d]**23:9** 2Fal 18:11; Hos 11:5; 2Fal 17:3-6; Yer 4:30
[e]**23:10** Hos 2:10; Eze 16:36, 41; Yer 42:10
[f]**23:11** Yer 3:8-11; Eze 16:51
[g]**23:12** 2Fal 16:7-15; 2Nya 28:16; Eze 16:15; 28
[h]**23:13** Hos 12:2; 2Fal 17:19
[i]**23:14** Eze 8:10; Nah 2:3; Yer 22:14
[j]14 *Wakaldayo* yaani *Wababeli.*
[k]**23:15** Isa 5:27
[l]15 *Ukaldayo* yaani *Babeli.*
[m]**23:16** Isa 57:9; Eze 6:9
[n]**23:17** Yer 40:9; Eze 16:29
[o]**23:18** Za 106:40; Yer 6:8; 12:8; Amo 5:21; Zek 11:8; Isa 57:8; Za 78:59
[p]**23:19** Eze 23:3
[q]**23:20** Eze 16:26
[r]**23:21** Eze 16:26
[s]**23:22** Yer 4:30; Eze 16:37
[t]**23:23** 2Fal 20:14-15; Yer 40:9; 50:21; 2Fal 24:2; Mwa 11:28
[u]**23:24** Yer 47:3; Nah 2:4; Yer 39:5-6; Eze 26:7-10

nao watakuadhibu sawasawa na sheria
zao. 25 [a]Nitaelekeza wivu wa hasira yangu
dhidi yako, nao watakushughulikia kwa
hasira kali. Watakatilia mbali pua yako
na masikio yako, na wale watakaosalia
miongoni mwako watauawa kwa upanga.
Watachukua wana wako na binti zako,
na wale watakaosalia miongoni mwenu
watateketezwa kwa moto. 26 [b]Watakuvua
pia nguo zako na kuchukua mapambo yako
yaliyotengenezwa kwa vito na dhahabu.
27 [c]Hivyo ndivyo nitakavyokomesha
uasherati wako na ukahaba wako uliouanza
huko Misri. Hutatazama vitu hivi kwa
kuvitamani tena, wala kukumbuka Misri
tena.
28 [d]"Kwa hiyo hili ndilo Bwana
Mwenyezi asemalo: Ninakaribia kukutia
mikononi mwa wale unaowachukia, kwa
wale uliojitenga nao kwa kuwachukia.
29 [e]Watakushughulikia kwa chuki na
kukunyang'anya kila kitu ulichokifanyia
kazi. Watakuacha uchi na mtupu na aibu
ya ukahaba wako itafunuliwa. Uasherati
wako na uzinzi wako 30 [f]umekuletea haya
yote, kwa sababu ulitamani mataifa na
kujinajisi kwa sanamu zao. 31 [g]Umeiendea
njia ya dada yako, hivyo nitakitia kikombe
chake mkononi mwako.
32 [h]"Hili ndilo Bwana Mwenyezi asemalo:

"Utakinywea kikombe cha dada
yako,
kikombe kikubwa na chenye kina
kirefu;
nitaletea juu yako dharau na
dhihaka,
kwa kuwa kimejaa sana.
33 [i]Utalewa ulevi na kujawa huzuni,
kikombe cha maangamizo na
ukiwa,
kikombe cha dada yako Samaria.
34 [j]Utakinywa chote na kukimaliza;
utakivunja vipande vipande
na kuyararua matiti yako.

Nimenena haya, asema Bwana Mwenyezi.
35 [k]"Kwa hiyo hili ndilo Bwana Mwenyezi
asemalo: Kwa kuwa tangu uliponisahau
mimi na kunitupa nyuma yako, lazima
ubebe matokeo ya uasherati wako na
ukahaba wako."
36 [l]Bwana akaniambia, "Mwanadamu,
Je, utawahukumu Ohola na Oholiba? Basi
wakabili kwa ajili ya matendo yao ya
machukizo, 37 [m]kwa kuwa wamefanya uzinzi
na damu imo mikononi mwao. Wamefanya
uzinzi na sanamu zao, hata wamewatoa
watoto wao walionizalia kuwa kafara,
kuwa chakula kwao. 38 [n]Pia wamenifanyia
hili: wakati huo huo wamenajisi patakatifu
pangu na kuzitangua Sabato zangu. 39 [o]Siku
ile ile walitoa watoto wao kuwa kafara kwa
sanamu zao, waliingia patakatifu pangu na
kupatia unajisi. Hilo ndilo walilolifanya
katika nyumba yangu.
40 [p]"Walituma hata wajumbe kuwaita
watu kutoka mbali, nao walipowasili
ulioga kwa ajili yao, ukapaka macho
yako rangi na ukavaa mapambo yako
yaliyotengenezwa kwa vito vya dhahabu.
41 [q]Ukaketi kwenye kiti cha anasa, kukiwa
na meza iliyoandaliwa mbele yake ambayo
juu yake ulikuwa umeweka uvumba na
mafuta ambayo yalikuwa yangu.

---

[a]**23:25** Eze 24:21; Yer 12:9; Eze 16:38; 20:47-48; Kum 29:20
[b]**23:26** Yer 13:22; Isa 3:18-23; Eze 16:39; Ufu 17:16
[c]**23:27** Eze 16:41; 22:15
[d]**23:28** Eze 34:20; Yer 21:7
[e]**23:29** Kum 28:48; Eze 16:36-39; 22:9; Yer 13:27; Mik 1:11
[f]**23:30** Za 106:37-38; Eze 6:9; Sef 3:1
[g]**23:31** Yer 25:15; 2Fal 21:13
[h]**23:32** Za 60:3; Isa 51:17; Eze 22:4-5; Yer 25:15; Hos 7:16; Za 44:13
[i]**23:33** Yer 25:15; Eze 12:19
[j]**23:34** Isa 51:17; Za 16:5; Yer 25:27
[k]**23:35** Yer 2:23; 3:21; Eze 22:12; 1Fal 14:9; Neh 9:26
[l]**23:36** Eze 16:2; Isa 58:1; Mik 3:8; Eze 22:2
[m]**23:37** Eze 16:36
[n]**23:38** Law 15:31; Neh 10:31
[o]**23:39** 2Fal 21:4; Yer 7:10; Eze 22:8
[p]**23:40** Yer 4:30; Isa 57:9; 2Fal 9:30; Hos 2:13; Eze 16:13-19
[q]**23:41** Mit 7:17; Amo 6:4; Isa 65:11; Eze 16:18-19; 41:22; 16:38; Hos 6:5

42 [a]"Kelele za umati wa watu wasiojali
zilikuwa zimemzunguka, wakaleta watu
wengi waliokuwa wakifanya makelele
na walevi kutoka nyikani, ambao walitia
bangili kwenye mikono ya yule mwanamke
na dada yake na pia taji nzuri za kupendeza
kwenye vichwa vyao. 43 [b]Ndipo nikasema
kuhusu yule aliyechakazwa na uzinzi, 'Basi
wamtumie kama kahaba, kwa kuwa ndivyo
alivyo.' 44 Nao wakazini naye. Kama vile
watu wazinivyo na kahaba, ndiyo hivyo
walivyozini na hao wanawake waasherati,
Ohola na Oholiba. 45 [c]Lakini watu wenye
haki, watawahukumia adhabu wanawake
wafanyao uzinzi na kumwaga damu, kwa
kuwa ni wazinzi na damu iko mikononi
mwao.

46 [d]"Hili ndilo BWANA Mwenyezi asemalo,
Leteni watu wengi wenye makelele dhidi
yao na uwaache wapate hofu na watekwe
nyara. 47 [e]Hao watu wengi watawapiga kwa
mawe na kuwaua kwa panga zao, watawaua
wana wao na binti zao na kuzichoma
nyumba zao.

48 [f]"Hivyo nitaukomesha uasherati katika
nchi, ili wanawake wote wapate onyo nao
wasije wakafanya uasherati kama ninyi
mlivyofanya. 49 [g]Utapata adhabu kwa ajili
ya uasherati wako na kuchukua matokeo ya
dhambi zako za uasherati. Ndipo utakapojua
kuwa Mimi ndimi BWANA Mwenyezi."

### *Chungu Cha Kupikia*

24 [h]Katika mwaka wa tisa, mwezi wa
kumi, siku ya kumi, neno la BWANA
likanijia kusema: 2 [i]"Mwanadamu, weka
kumbukumbu ya tarehe hii, tarehe hii hasa,
kwa kuwa mfalme wa Babeli ameuzingira
mji wa Yerusalemu kwa jeshi siku hii ya
leo. 3 [j]Iambie nyumba hii ya kuasi fumbo,
na uwaambie, 'Hili ndilo BWANA Mwenyezi
asemalo:

" 'Teleka sufuria jikoni; iteleke
na umimine maji ndani yake,
4 [k]Weka vipande vya nyama ndani
yake,
vipande vyote vizuri,
vya paja na vya bega.
Ijaze hiyo sufuria kwa mifupa hii
mizuri;
5 [l]chagua yule aliye bora wa kundi
la kondoo.
Panga kuni chini ya sufuria kwa ajili
ya mifupa;
chochea mpaka ichemke
na uitokose hiyo mifupa ndani
yake.

6 [m]" 'Kwa kuwa hili ndilo BWANA
Mwenyezi asemalo:

" 'Ole wa mji umwagao damu,
ole wa sufuria ambayo sasa
ina ukoko ndani yake,
ambayo ukoko wake hautoki.
Kipakue kipande baada ya kipande,
bila kuvipigia kura.

7 [n]" 'Kwa kuwa damu aliyoimwaga ipo
katikati yake:
huyo mwanamke aliimwaga
juu ya mwamba ulio wazi;
hakuimwaga kwenye ardhi,
ambako vumbi lingeifunika.
8 [o]Kuchochea ghadhabu na kulipiza
kisasi,
nimemwaga damu yake
juu ya mwamba ulio wazi,
ili isifunikwe.

9 [p]" 'Kwa hiyo, hili ndilo BWANA Mwenyezi
asemalo:

---

[a]**23:42** Za 73:5; 2Nya 9:1; Mwa 24:30; Eze 16:11-12
[b]**23:43** Eze 23:3
[c]**23:45** Eze 16:38
[d]**23:46** Eze 16:40
[e]**23:47** Yer 34:22; Eze 16:40-41; 2Nya 36:17-19
[f]**23:48** Eze 22:15; Kum 13:11; 2Pet 2:6
[g]**23:49** Isa 9:10; Eze 16:58; 24:13; 20:38
[h]**24:1** Eze 8:1; 26:1; 29:17
[i]**24:2** 2Fal 25:1; Yer 52:4; Isa 30:8; Hab 2:2; Yer 39:1
[j]**24:3** Za 78:2; Eze 17:2; 11:3-6; 11:3
[k]**24:4** Eze 11:7
[l]**24:5** Isa 34:12; Yer 52:10, 24-27; Mik 3:2-3
[m]**24:6** Eze 22:2; Ay 6:27; Nah 3:10; Oba 1:11; Eze 16:23; Yoe 3:3; Eze 11:11
[n]**24:7** Law 17:13; Kum 12:16
[o]**24:8** Mt 7:2
[p]**24:9** Eze 24:6; Nah 3:1; Hab 2:12

" 'Ole wa mji umwagao damu!
Mimi nami nitalundikia kuni
nyingi.
10 Kwa hiyo lundika kuni
na uwashe moto.
Pika hiyo nyama vizuri,
changanya viungo ndani yake,
na uiache mifupa iungue kwenye
moto.
11 [a]Kisha teleka sufuria tupu kwenye
makaa
mpaka iwe na moto sana na shaba
yake ing'ae,
ili uchafu wake upate kuyeyuka
na ukoko wake upate kuungua na
kuondoka.
12 Imezuia juhudi zote,
ukoko wake mwingi haujaondoka,
hata ikiwa ni kwa moto.

13 [b]" 'Sasa uchafu wako ni uasherati
wako. Kwa sababu nilijaribu kukutakasa
lakini haikuwezekana kutakaswa kutoka
kwenye huo uchafu wako, hutatakasika
tena mpaka ghadhabu yangu dhidi yako
iwe imepungua.
14 [c]" 'Mimi Bwana nimesema, wakati
umewadia wa mimi kutenda. Mimi sitazuia,
mimi sitaona huruma wala sitapunguza
hasira yangu, Utahukumiwa sawasawa
na mwenendo na matendo yako, asema
Bwana Mwenyezi.' "

*Kifo Cha Mke Wa Ezekieli*

15 Neno la Bwana likanijia kusema:
16 [d]"Mwanadamu, kwa pigo moja nakaribia
kukuondolea kile kilicho furaha ya macho
yako. Lakini usiomboleze au kulia wala
kudondosha machozi yoyote. 17 [e]Lia kwa
uchungu kimya kimya usimwombolezee
mtu aliyekufa. Jifunge kilemba chako
na uvae viatu vyako miguuni mwako,
usifunike sehemu ya chini ya uso wako,
wala usile vyakula vya kawaida vya wakati
wa matanga."
18 [f]Hivyo nikanena na watu asubuhi
na jioni mke wangu akafa. Asubuhi yake
nilifanya kama nilivyoamriwa.
19 [g]Ndipo watu wakaniuliza, "Je, jambo
hili unalofanya linamaanisha nini kwetu?"
20 Kwa hiyo nikawaambia, "Neno la
Bwana lilinijia kusema: 21 [h]"Sema na nyumba
ya Israeli. Hili ndilo Bwana Mwenyezi
asemalo: Ninakaribia kupatia unajisi
mahali pangu patakatifu, ngome ambayo
ndani yake mnaona fahari, furaha ya macho
yenu, kitu mnachokipenda. Wana wenu na
binti zenu mliowaacha nyuma wataanguka
kwa upanga. 22 [i]Nanyi mtafanya kama
nilivyofanya. Hamtafunika sehemu ya chini
ya nyuso zenu wala hamtakula vyakula vya
kawaida vya waombolezaji. 23 [j]Mtajifunga
vilemba vichwani mwenu na kuvaa viatu
vyenu miguuni mwenu. Hamtaomboleza au
kulia, lakini mtadhoofika kwa sababu ya
dhambi zenu na kulia kwa uchungu kila mtu
na mwenzake. 24 [k]Ezekieli atakuwa ishara
kwenu, mtafanya kama yeye alivyofanya.
Wakati jambo hili litakapotokea, mtajua
kuwa Mimi ndimi Bwana Mwenyezi.'
25 [l]"Nawe, mwanadamu, siku ile
nitakapoondoa ngome yao iliyo furaha
yao na utukufu wao, kitu cha kupendeza
macho yao, kile kilicho shauku ya mioyo
yao, wana wao na binti zao vilevile, 26 [m]siku
hiyo atakayetoroka atakuja kuwapasha
habari. 27 [n]Katika siku ile kinywa chako
kitamfumbukia yeye aliyenusurika, nawe
utaongea wala hutanyamaza tena. Hivyo
wewe utakuwa ishara kwao, nao watajua
kuwa Mimi ndimi Bwana."

[a]**24:11** Yer 21:10; Eze 22:15
[b]**24:13** Mao 1:9; Zek 6:8; Eze 5:13; 8:18; Isa 22:14; Yer 6:28-30; Eze 16:18
[c]**24:14** Zek 8:14; Hes 23:19; Isa 3:11; Eze 18:30; Isa 22:14; Hes 11:23; Ay 27:22
[d]**24:16** Yer 13:17; 16:5; Za 39:10; 84:1; Mao 2:4; Yer 22:10
[e]**24:17** Yer 16:7; Hes 20:29; Isa 3:20; 20:2; 20:2; Law 13:45
[f]**24:18** Eze 12:7
[g]**24:19** Eze 12:9; 37:18
[h]**24:21** Za 27:4; Yer 7:14; Eze 23:25; Hos 9:12-16; Mal 2:12; Law 26:19, 31
[i]**24:22** Yer 16:7; Law 13:45
[j]**24:23** Kut 33:4; Ay 27:15; Za 78:64; Kut 28:39; Isa 3:20
[k]**24:24** Isa 20:3; Eze 4:3; Yn 13:19; Eze 12:11
[l]**24:25** Kum 28:32; Yer 11:22; Za 20:4; Mao 2:4
[m]**24:26** 1Sam 4:12; Ay 1:15-19
[n]**24:27** Eze 3:26; 33:22; Dan 10:15

*Unabii Dhidi Ya Amoni*

25 Neno la BWANA likanijia kusema:
2 [a]“Mwanadamu, elekeza uso wako juu
ya Waamoni utabiri dhidi yao. 3 [b]Waambie,
‘Sikieni neno la BWANA Mwenyezi. Hili
ndilo BWANA Mwenyezi asemalo: Kwa
sababu ulisema, “Aha!” juu ya mahali
pangu patakatifu palipotiwa unajisi, na juu
ya nchi ya Israeli ilipoangamizwa, na juu ya
watu wa Yuda walipokwenda uhamishoni,
4 [c]kwa hiyo nitawatia mikononi mwa watu
wa mashariki mkawe mali yao. Watapiga
kambi zao katikati yenu na kufanya makazi
miongoni mwenu, watakula matunda yenu
na kunywa maziwa yenu. 5 [d]Nitaufanya mji
wa Raba kuwa malisho ya ngamia na Amoni
kuwa mahali pa kondoo pa kupumzikia.
Ndipo mtakapojua kuwa Mimi ndimi
BWANA. 6 [e]Kwa kuwa hili ndilo BWANA
Mwenyezi asemalo: Kwa kuwa umepiga
makofi yako na kufanya kishindo kwa
miguu, mkifurahia kwa mioyo yenu miovu
juu ya yale mabaya yaliyoipata nchi ya
Israeli, 7 [f]hivyo nitaunyoosha mkono
wangu dhidi yako na kukutoa kuwa nyara
kwa mataifa. Nitakukatilia mbali kutoka
kwenye mataifa na kukung’oa katika nchi.
Nitakuangamiza, nawe utajua ya kuwa
Mimi ndimi BWANA.’ ”

*Unabii Dhidi Ya Moabu*

8 [g]“Hili ndilo BWANA Mwenyezi asemalo:
‘Kwa sababu Moabu na Seiri wamesema,
“Tazama, nyumba ya Yuda imekuwa
kama mataifa mengine yote,” 9 [h]kwa hiyo
nitaiondoa ile miji iliyo kando ya
Moabu, kuanzia miji iliyoko mipakani,
yaani: Beth-Yeshimothi, Baal-Meoni na
Kiriathaimu, iliyo utukufu wa nchi hiyo.
10 [i]Nitaitia Moabu pamoja na Waamoni
mikononi mwa watu wa Mashariki
kuwa milki yao, ili kwamba Waamoni
wasikumbukwe miongoni mwa mataifa,
11 [j]nami nitatoa adhabu kwa Moabu. Ndipo
watakapojua kuwa Mimi ndimi BWANA.’ ”

*Unabii Dhidi Ya Edomu*

12 [k]“Hili ndilo BWANA Mwenyezi asemalo:
‘Kwa sababu Edomu ulilipiza kisasi juu
ya nyumba ya Yuda na kukosa sana kwa
kufanya hivyo, 13 [l]kwa hiyo hili ndilo
BWANA Mwenyezi asemalo: Nitaunyoosha
mkono wangu dhidi ya Edomu na kuua watu
wake na wanyama wao. Nitaufanya ukiwa,
kuanzia Temani hadi Dedani wataanguka
kwa upanga. 14 [m]Nitalipiza Edomu kisasi
kwa mkono wa watu wangu Israeli, nao
watawatendea Edomu sawasawa na hasira
yangu na ghadhabu yangu, nao watakijua
kisasi changu, asema BWANA Mwenyezi.’ ”

*Unabii Dhidi Ya Ufilisti*

15 [n]“Hili ndilo BWANA Mwenyezi asemalo:
‘Kwa sababu Wafilisti wamewalipiza kisasi
kwa uovu wa mioyo yao na kwa uadui wa
siku nyingi wakataka kuangamiza Yuda,
16 [o]kwa hiyo hili ndilo BWANA Mwenyezi
asemalo: Mimi ninakaribia kuunyoosha
mkono wangu dhidi ya Wafilisti, nami
nitawakatilia mbali Wakerethi na
kuwaangamiza wale waliosalia katika
pwani. 17 [p]Nitalipiza kisasi kikubwa juu yao
na kuwaadhibu katika ghadhabu yangu.
Ndipo watakapojua kuwa Mimi ndimi
BWANA, nitakapolipiza kisasi juu yao.’ ”

[a]**25:2** Sef 2:9; Eze 21:28; Yer 49:1-6; Eze 13:17; 29:2
[b]**25:3** Za 35:21; Eze 36:2; Mit 17:5; Sef 2:9; Eze 36:2
[c]**25:4** Mwa 25:6; Amu 6:3-33; Kum 28:33; Mwa 45:18; Hes 31:10
[d]**25:5** Kum 3:11; Isa 17:2; Eze 21:20; Sef 2:14
[e]**25:6** Mao 1:12; Sef 2:8; Eze 6:11; Hes 24:10
[f]**25:7** Eze 21:31; Amo 1:14-15; Hes 14:3; Eze 13:14-17
[g]**25:8** Mwa 19:37; Yer 48:1; Kum 23:6; Isa 16:6; Mwa 14:6
[h]**25:9** Yos 13:19; Hes 32:3, 37; Yos 13:17; Hes 33:49
[i]**25:10** Eze 25:4; 21:32
[j]**25:11** Isa 15:9; Yer 48:9; Isa 16:1-14
[k]**25:12** 2Sam 8:13-14; Mao 4:22; Oba 1:10; Isa 11:14; 2Nya 28:17
[l]**25:13** Eze 29:8; Yer 25:23; Kut 7:5; Eze 16:27; Yer 49:10; Eze 14:17; Mwa 36:11-15
[m]**25:14** Eze 32:29; 35:2-3, 11; 36:5
[n]**25:15** Yer 25:20; 47:1; Yoe 3:4; Amo 1:6; 2Nya 28:18
[o]**25:16** 2Nya 26:6; Yer 47:1-7; 1Sam 30:14; Eze 20:33
[p]**25:17** Hes 31:3; Yer 44:13; Kut 6:2; 8:22; Isa 11:14; 14:30; Yer 47:7; Yoe 3:4

*Unabii Dhidi Ya Tiro*

26 [a]Mwaka wa kumi na moja, siku ya
kwanza ya mwezi, neno la BWANA
likanijia kusema: 2 [b]“Mwanadamu, kwa
sababu Tiro amesema kuhusu Yerusalemu,
‘Aha! Lango la kwenda kwa mataifa
limevunjika, nayo milango yake iko wazi
mbele yangu, sasa kwa kuwa amekuwa
magofu nitastawi.’ 3 [c]Kwa hiyo hili
ndilo BWANA Mwenyezi asemalo: Mimi
niko kinyume na wewe, ee Tiro, nami
nitaleta mataifa mengi dhidi yako, kama
bahari inayovurumisha mawimbi yake.
4 [d]Watavunja kuta za Tiro na kuibomoa
minara yake, nitakwangua udongo wake
na kuufanya mwamba mtupu. 5 [e]Itakuwa
huko katikati ya bahari patakuwa mahali
pa kutandaza nyavu za kuvulia samaki, kwa
maana nimenena, asema BWANA Mwenyezi.
Atakuwa nyara kwa mataifa, 6 [f]nayo makao
yake huko bara yataangamizwa kwa
upanga. Ndipo watakapojua kwamba Mimi
ndimi BWANA.

7 [g]“Kwa maana hili ndilo BWANA
Mwenyezi asemalo: Kutoka kaskazini
nitamleta dhidi ya Tiro Mfalme Nebukadneza
wa Babeli, mfalme wa wafalme, akiwa na
farasi na magari ya vita, wapanda farasi na
jeshi kubwa. 8 [h]Atayaharibu makao yako
huko bara kwa upanga, ataweka jeshi
kukuzingira, atakuzingira mpaka kwenye
kuta za ngome zako na kuinua ngao zake
dhidi yako. 9 [i]Ataelekeza mapigo ya vyombo
vyake vya kubomolea dhidi ya kuta zako
na kubomoa minara yako kwa silaha
zake. 10 [j]Farasi zake zitakuwa nyingi sana
kiasi kwamba utafunikwa na mavumbi
watakayotimua. Kuta zako zitatikisika kwa
mshindo wa farasi wa vita, magari makubwa
na magari ya vita wakati aingiapo malango
yako kama watu waingiao mji ambao kuta
zake zimebomolewa kote.

11 [k]“Kwato za farasi zake zitakanyaga
barabara zako zote, atawaua watu wako
kwa upanga na nguzo zako zilizo imara
zitaanguka chini. 12 [l]Watateka utajiri
wako na kuchukua nyara bidhaa zako,
watazivunja kuta zako na kuzibomoa
nyumba zako nzuri, watatupa baharini
mawe yako, mbao zako na kifusi chako.
13 [m]Nitakomesha kelele za nyimbo zako, na
uimbaji wako wa kinubi kamwe hautasikika
tena. 14 [n]Nitakufanya mwamba mtupu, nawe
utakuwa mahali pa kutandazia nyavu za
kuvulia samaki. Kamwe hutajengwa tena,
kwa maana Mimi BWANA nimenena, asema
BWANA Mwenyezi.

15 [o]“Hili ndilo BWANA Mwenyezi asemalo
kwa Tiro: ‘Je, nchi za pwani hazitatetemeka
kwa kishindo cha anguko lako, wakati
majeruhi wanapolia kwa maumivu makali
na wakati mauaji yanaendelea ndani
yako? 16 [p]Ndipo wakuu wote wa mataifa
ya pwani watashuka kutoka kwenye viti
vyao vya enzi na kuweka kando majoho
yao na kuvua nguo zao zilizotariziwa.
Wakiwa wamevikwa hofu kuu, wataketi
chini ardhini, wakiwa wanatetemeka kila
dakika na wakikustajabia. 17 [q]Ndipo wao
watakuombolezea na kukuambia:

“ ‘Tazama jinsi ulivyoharibiwa,
ee mji uliokuwa na sifa,
wewe uliyekaliwa na mabaharia!
Ulikuwa na nguvu kwenye bahari,
wewe na watu wako;
wote walioishi huko,
uliwatia hofu kuu.

---

[a]**26:1** Eze 24:1; 29:1; 30:20
[b]**26:2** Yos 19:29; 2Sam 5:11; Eze 25:3; Yoe 3:4-6
[c]**26:3** Isa 5:30; Yer 50:42; 51:42
[d]**26:4** Isa 23:1, 11; Amo 1:10
[e]**26:5** Eze 27:32; Hes 14:3; Eze 29:19; Mt 4:19-21; Eze 47:10; Zek 9:2-4
[f]**26:6** Eze 25:5
[g]**26:7** Yer 27:6; Ezr 7:12; Dan 2:37; Nah 2:3-4; Eze 23:24
[h]**26:8** Yer 6:6; 33:4; Eze 21:22; 2Sam 20:15
[i]**26:9** Eze 21:22
[j]**26:10** Yer 4:13; 46:9; Eze 23:24
[k]**26:11** Isa 5:28; Yer 43:13; Isa 26:5
[l]**26:12** Yer 4:7; Hab 1:8; Isa 23:8; Eze 27:3-27
[m]**26:13** Yer 7:34; Za 137:2; Isa 14:11; Ay 30:31; Ufu 18:22; Hos 2:11
[n]**26:14** Ay 12:14; Mal 1:4
[o]**26:15** Isa 41:5; Eze 27:35; Yer 49:21; Ay 24:12
[p]**26:16** Ay 8:22; Hos 11:10; Isa 3:26; Eze 32:10; Kut 26:36; Ay 2:8-13; Law 26:32
[q]**26:17** Eze 19:1; Isa 14:12

18 [a]Sasa nchi za pwani zinatetemeka
katika siku ya anguko lako;
visiwa vilivyomo baharini
vinaogopa kwa kuporomoka
kwako.'

19 [b]"Hili ndilo BWANA Mwenyezi asemalo:
Nitakapokufanya uwe mji wa ukiwa, kama
miji isiyokaliwa tena na watu, nitakapoleta
vilindi vya bahari juu yako na maji yake
makuu yatakapokufunika, 20 [c]ndipo
nitakapokushusha chini pamoja na wale
washukao shimoni, kwa watu wa kale, nami
nitakufanya uishi katika pande za chini za
nchi kama katika magofu ya kale, pamoja
na wale washukao shimoni, nawe hutarudi
au kurejea kwenye makao yako katika nchi
ya walio hai. 21 [d]Nitakufikisha mwisho
wa kutisha wala hutakuwepo tena. Watu
watakutafuta, lakini kamwe hutaonekana
tena, asema BWANA Mwenyezi."

*Maombolezo Kwa Ajili Ya Tiro*

27 Neno la BWANA likanijia kusema:
2 [e]"Mwanadamu, fanya maombolezo
kwa ajili ya Tiro. 3 [f]Umwambie Tiro, ulioko
kwenye lango la bahari, ufanyao biashara
na mataifa mengi ya pwani, 'Hili ndilo
BWANA Mwenyezi asemalo:

" 'Ee Tiro, wewe umesema,
"Mimi ni mkamilifu katika uzuri."
4 [g]Mipaka yako ilikuwa katika moyo
wa bahari,
wajenzi wako walikamilisha uzuri
wako.
5 [h]Walizifanya mbao zako zote
kwa misunobari itokayo Seniri;[i]
walichukua mierezi kutoka Lebanoni
kukutengenezea mlingoti.
6 [j]Walichukua mialoni toka Bashani
wakakutengenezea makasia yako;
kwa miti ya msanduku
kutoka pwani ya Kitimu
wakatengeneza sitaha[k] yako
na kuipamba kwa pembe za
ndovu.
7 [l]Kitani safi kilichotariziwa kutoka
Misri kilikuwa tanga lako,
nacho kilikuwa bendera yako;
chandarua chako kilikuwa cha rangi
ya buluu na ya zambarau
kutoka visiwa vya Elisha.
8 [m]Watu kutoka Sidoni na Arvadi
walikuwa wapiga makasia
yako;
watu wako wenye ustadi, ee Tiro,
walikuwa ndio mabaharia wako.
9 [n]Wazee wa Gebali[o] pamoja na
mafundi stadi
walikuwa mafundi wako melini.
Meli zote za baharini na mabaharia
wao
walikuja kwako ili kubadilishana
bidhaa zako.

10 [p]" 'Watu wa Uajemi, Ludi na Putu
walikuwa askari katika jeshi lako.
Walitundika ngao zao na chapeo zao
kwenye kuta zako,
wakileta fahari yako.
11 [q]Watu wa Arvadi na wa Heleki
walikuwa juu ya kuta zako pande
zote;
watu wa Gamadi
walikuwa kwenye minara yako.

---

[a]**26:18** Isa 23:5; 41:5; Za 46:6; Yer 49:21; Eze 27:35
[b]**26:19** Isa 8:7-8; Mwa 7:11
[c]**26:20** Amo 9:2; Yon 2:2-6; Ay 28:13; Isa 14:9-10; Eze 32:18; Ay 28:13; Hes 16:30
[d]**26:21** Yer 20:4; Ufu 18:21; Za 37:36; Yer 51:64; Dan 11:19
[e]**27:2** Eze 19:1; 26:17; 28:12; 32:2
[f]**27:3** Hos 9:13; Isa 23:9; Eze 28:2; Za 83:16
[g]**27:4** Eze 28:12
[h]**27:5** Kum 3:9; Isa 2:13
[i]5 Yaani Hermoni.
[j]**27:6** Za 29:9; Zek 11:2; Mwa 10:4; Isa 23:12; Yer 22:20; Hes 21:33
[k]6 Yaani sakafu ya merikebu au mashua.
[l]**27:7** Kut 25:4; Yer 10:9; Isa 19:9; Mwa 10:4; Kut 26:36
[m]**27:8** Mwa 10:18; 1Fal 9:23-27
[n]**27:9** Yos 13:5; 1Fal 5:18; Za 104:26
[o]9 Yaani Bubilo, mji wa zamani sana wa Ufoinike (kama kilomita 80 kaskazini mwa Beiruti).
[p]**27:10** Dan 8:20; Mwa 10:6; Nah 3:9; Yer 46:9; Eze 38:5; 2Nya 36:20; Isa 66:19; Wim 4:4
[q]**27:11** Eze 27:27

Walitundika ngao zao kuzizunguka
kuta zako;
wakaukamilisha uzuri wako.

12 [a]“ ‘Tarshishi walifanya biashara nawe
kwa sababu ya utajiri wako mkubwa wa
bidhaa, walibadilisha fedha, chuma, bati
na risasi kwa mali zako.
13 [b]“ ‘Uyunani, Tubali na Mesheki,
walifanya biashara nawe, walibadilisha
watumwa na vyombo vya shaba kwa bidhaa
zako.
14 [c]“ ‘Watu wa Beth-Togarma walibadilisha
farasi wa mizigo, farasi wa vita na nyumbu
kwa mali zako.
15 [d]“ ‘Watu wa Dedani[e] walifanya biashara
nawe, watu wengi wa nchi za pwani
walikuwa wachuuzi wako, walikulipa kwa
pembe za ndovu na mpingo.
16 [f]“ ‘Watu wa Aramu walifanya biashara
nawe kwa ajili ya wingi wa kazi za mikono
yako, wakibadilishana kwa almasi,
vitambaa vya rangi ya zambarau, vitambaa
vilivyotariziwa, kitani safi, matumbawe[g] na
akiki nyekundu.
17 [h]“ ‘Yuda na Israeli walifanya biashara
nawe, walibadilishana kwa ngano kutoka
Minithi, mtama, asali, mafuta na zeri ya
kuponyeshea.
18 [i]“ ‘Dameski, kwa sababu ya wingi
wa kazi za mikono yako na ukuu wa
utajiri wa mali, walifanya biashara nawe
wakibadilishana mvinyo kutoka Helboni
na sufu kutoka Zahari.
19 [j]“ ‘Wadani na Wayunani kutoka
Uzali, walikuletea mali za biashara, nao
wakabadilishana nawe chuma kilichofuliwa,
mdalasini na mchaichai.
20 [k]“ ‘Dedani alifanya biashara nawe kwa
matandiko ya farasi.
21 [l]“ ‘Arabuni na wakuu wote wa Kedari
walikuwa wanunuzi wako waliobadilishana
bidhaa zako na wana-kondoo, kondoo dume
na mbuzi.
22 [m]“ ‘Wafanyabiashara wa Sheba na
wa Raama walifanya biashara nawe,
wakabadilishana bidhaa zako na aina zote
za vikolezi, vito vya thamani na dhahabu.
23 [n]“ ‘Harani, Kane na Edeni na
wafanyabiashara wa Sheba, Ashuru na
Kilmadi walifanya biashara nawe. 24 Kwenye
soko lako, walifanya biashara nawe kwa
mavazi mazuri, vitambaa vya buluu,
nguo za kutariziwa na mazulia ya rangi
mbalimbali yenye kamba zilizosokotwa na
kuwekwa mafundo imara.

25 [o]“ ‘Merikebu za Tarshishi ndizo
zinazokusafirishia bidhaa zako.
Umejazwa shehena kubwa
katika moyo wa bahari.
26 [p]Wapiga makasia wako
wanakupeleka
mpaka kwenye maji makavu.
Lakini upepo wa mashariki
umekuvunja vipande vipande
katika moyo wa bahari.
27 [q]Utajiri wako, bidhaa zako na mali
zako,
mabaharia wako, manahodha
wako,
mafundi wako wa meli,
wafanyabiashara wako na askari
wako wote,
na kila mmoja aliyeko melini

[a]**27:12** Mwa 10:4; 2Nya 20:36
[b]**27:13** Isa 66:19; Ufu 18:13; Yoe 3:6; Mwa 10:2; Eze 32:26; 38:2
[c]**27:14** Mwa 10:3; Eze 38:6
[d]**27:15** Mwa 10:7; Yer 25:22; 1Fal 10:22; Ufu 18:12
[e]15 Yaani *Rhodes*.
[f]**27:16** Amu 10:6; Isa 7:1-8; Kut 28:18; 39:11; Eze 28:13; 16:10; Ay 28:18
[g]16 Yaani marijani, jiwe laini la pwani au baharini, kama mawe ya chokaa.
[h]**27:17** Amu 11:33; Mdo 12:20; Mwa 43:11
[i]**27:18** Mwa 14:15; Eze 47:16-18
[j]**27:19** Kut 30:24; Mwa 10:2, 27
[k]**27:20** Mwa 10:7
[l]**27:21** Mwa 25:13; Isa 60:7; 2Nya 9:14; Isa 21:17
[m]**27:22** 1Fal 10:1-2; Isa 60:8; Mwa 43:11; Za 72:10; Ufu 18:12
[n]**27:23** Mwa 11:26; 2Fal 19:12; Isa 37:12; Mwa 10:22; Hes 24:24
[o]**27:25** Mwa 10:4; Isa 2:16; Ufu 18:3
[p]**27:26** Mwa 41:6; Za 48:7; Yer 18:7
[q]**27:27** Mit 11:4; Eze 28:8

atazama kwenye moyo wa bahari
siku ile ya kuvunjika kwa meli
yako.
28 [a]Nchi za pwani zitatetemeka
wakati mabaharia wako
watakapopiga kelele.
29 [b]Wote wapigao makasia
wataacha meli zao,
mabaharia wote na wanamaji wote
watasimama pwani.
30 [c]Watapaza sauti zao
na kulia sana kwa ajili yako;
watajitupia mavumbi juu ya vichwa
vyao
na kujivingirisha kwenye majivu.
31 [d]Watanyoa nywele zao kwa ajili
yako,
nao watavaa nguo za magunia.
Watakulilia kwa uchungu wa moyo
na kwa maombolezo makuu.
32 [e]Watakapokuwa wanalia na
kuomboleza juu yako,
watafanya maombolezo kukuhusu
wakisema:
"Ni nani aliyepata kuangamizwa
kama Tiro,
katika moyo wa bahari?"
33 [f]Wakati bidhaa zako zilipotoka
baharini,
ulitosheleza mataifa mengi;
kwa wingi wa utajiri wako na bidhaa
zako
ulitajirisha wafalme wa dunia.
34 [g]Sasa umevunjavunjwa na bahari,
katika vilindi vya maji,
bidhaa zako na kundi lako lote
vimezama pamoja nawe.
35 [h]Wote waishio katika nchi za pwani
wanakustaajabia;
wafalme wao wanatetemeka kwa
hofu kuu,
nazo nyuso zao zimekunjamana
kwa woga.
36 [i]Wafanyabiashara miongoni mwa
mataifa wanakucheka;
umefikia mwisho wa kutisha
nawe hutakuwepo tena.' "

*Unabii Dhidi Ya Mfalme Wa Tiro*

28 Neno la BWANA likanijia kusema:
2 [j]"Mwanadamu, mwambie mfalme wa
Tiro, 'Hili ndilo BWANA Mwenyezi asemalo:

" 'Kwa sababu moyo wako umejivuna
na umesema, "Mimi ni mungu;
nami ninaketi katika kiti cha enzi
cha mungu
katika moyo wa bahari."
Lakini wewe ni mwanadamu, wala si
mungu,
ingawa unafikiri kuwa una hekima
kama mungu.
3 [k]Je, wewe una hekima kuliko
Danieli?
Je, hakuna siri iliyofichika kwako?
4 [l]Kwa hekima yako na ufahamu wako,
umejipatia utajiri,
nawe umejikusanyia dhahabu
na fedha katika hazina zako.
5 [m]Kwa werevu wako mwingi katika
biashara,
umeongeza utajiri wako
na kwa sababu ya utajiri wako
moyo wako umekuwa na kiburi.

6 " 'Kwa hiyo, hili ndilo BWANA Mwenyezi
asemalo:

" 'Kwa sababu unafikiri una hekima,
mwenye hekima kama mungu,

[a]**27:28** Yer 49:21; Eze 26:15
[b]**27:29** Ufu 18:17
[c]**27:30** Yos 7:6; Yer 6:26; Ufu 18:17-19; Mao 2:10
[d]**27:31** Isa 16:9; Ay 3:20; Es 4:1; Law 13:40; Ay 1:20; Isa 3:17; Yer 48:37; Isa 22:12; Mao 2:10; Eze 7:16
[e]**27:32** Eze 19:1; 26:17; Isa 23:1-6
[f]**27:33** Eze 28:4-5
[g]**27:34** Za 9:4
[h]**27:35** Eze 26:15; Law 26:32; Ay 18:20; Eze 32:10
[i]**27:36** Yer 18:16; Sef 2:15; Eze 26:21; Za 37:10; Yer 19:8; 49:17; 50:13
[j]**28:2** Isa 14:13; Mwa 3:4-5; 2The 2:4; Kum 8:14; Mit 16:18; Sef 2:15; Za 9:20
[k]**28:3** Dan 1:20; 2:20-23, 28; Zek 9:2; Eze 14:14
[l]**28:4** Zek 9:3; Isa 10:13
[m]**28:5** Ay 31:25; Hos 13:6; Kum 8:12-14; Isa 23:8; Yer 9:23; 9:23; Eze 27:33

7 [a]mimi nitawaleta wageni dhidi yako,
taifa katili kuliko yote;
watafuta panga zao dhidi ya uzuri
wa hekima yako,
na kuchafua fahari yako
inayong'aa.
8 [b]Watakushusha chini shimoni,
nawe utakufa kifo cha kikatili
katika moyo wa bahari.
9 [c]Je, wakati huo utasema, "Mimi ni
mungu,"
mbele ya wale wanaokuua?
Utakuwa mwanadamu tu, wala si
mungu,
mikononi mwa hao wanaokuua.
10 [d]Utakufa kifo cha wasiotahiriwa
kwa mkono wa wageni.

Kwa kuwa mimi nimenena, asema BWANA Mwenyezi.' "

11 Neno la BWANA likanijia kusema:
12 [e]"Mwanadamu, mfanyie maombolezo mfalme wa Tiro, nawe umwambie: 'Hili ndilo BWANA Mwenyezi asemalo:

" 'Ulikuwa kipeo cha ukamilifu,
ukiwa umejaa hekima
na mkamilifu katika uzuri.
13 [f]Ulikuwa ndani ya Edeni,
bustani ya Mungu;
kila kito cha thamani kilikupamba:
akiki nyekundu, yakuti manjano
na zumaridi,
krisolitho, shohamu na yaspi,
yakuti samawi, almasi na
zabarajadi.
Kuwekwa kwa hayo mapambo na
kushikizwa kwake
kulifanywa kwa dhahabu;
siku ile ulipoumbwa yaliandaliwa
tayari.
14 [g]Ulitiwa mafuta kuwa kerubi mlinzi,
kwa kuwa hivyo ndivyo
nilivyokuweka wakfu.
Ulikuwa kwenye mlima mtakatifu
wa Mungu;
ulitembea katikati ya vito vya
moto.
15 Ulikuwa mnyofu katika njia zako
tangu siku ile ya kuumbwa kwako,
hadi uovu ulipoonekana ndani
yako.
16 [h]Kutokana na biashara yako
iliyoenea,
ulijazwa na dhuluma,
nawe ukatenda dhambi.
Hivyo nilikuondoa kwa aibu kutoka
mlima wa Mungu,
nami nikakufukuza, ee kerubi
mlinzi,
kutoka katikati ya vito vya moto.
17 [i]Moyo wako ukawa na kiburi
kwa ajili ya uzuri wako,
nawe ukaiharibu hekima yako
kwa sababu ya fahari yako.
Kwa hiyo nikakutupa chini;
nimekufanya kioja mbele ya
wafalme.
18 [j]Kwa dhambi zako nyingi na
biashara yako ya dhuluma,
umenajisi mahali pako patakatifu.
Kwa hiyo nilifanya moto utoke ndani
yako,
nao ukakuteketeza,
nami nikakufanya majivu juu ya
nchi,
machoni pa wote waliokuwa
wakitazama.
19 [k]Mataifa yote yaliyokujua
yanakustajabia;
umefikia mwisho wa kutisha
na hutakuwepo tena milele.' "

*Unabii Dhidi Ya Sidoni*

20 Neno la BWANA likanijia kusema:

[a]**28:7** Eze 32:12; 30:11; 31:12; Yer 9:23; Eze 7:24
[b]**28:8** Za 55:23; Eze 32:30; 27:27; 26:12; Ufu 18:7
[c]**28:9** Isa 31:3; Eze 16:49
[d]**28:10** 1Sam 14:6; Yer 9:26; Eze 32:18-19
[e]**28:12** Eze 19:1; 27:2-4
[f]**28:13** Mwa 2:8; Eze 31:8-9; 27:16; Ufu 17:4; Isa 14:11; Ufu 21:20
[g]**28:14** Kut 30:26; 40:9; 25:17-20
[h]**28:16** Mwa 6:11; Hab 2:17; Mwa 3:24
[i]**28:17** Isa 10:12; Eze 16:49; 31:10; 19:12
[j]**28:18** Oba 1:18; Mal 4:3; Zek 9:2-4
[k]**28:19** Yer 51:64; Eze 26:21; Law 26:21

21 [a]"Mwanadamu, elekeza uso wako juu ya
Sidoni, ukatabiri dhidi yake, 22 [b]nawe useme:
'Hili ndilo BWANA Mwenyezi asemalo:

" 'Mimi ni kinyume chako, ee Sidoni,
nami nitapata utukufu ndani yako.
Nao watajua kwamba Mimi ndimi BWANA,
nitakapotekeleza hukumu zangu
na kuonyesha utakatifu wangu ndani yake.
23 [c]Nitapeleka tauni ndani yake
na kufanya damu itiririke katika barabara zake.
Waliochinjwa wataanguka ndani yake,
kwa upanga dhidi yake kila upande.
Ndipo watakapojua kwamba Mimi ndimi BWANA.

24 [d]" 'Nyumba ya Israeli hawatakuwa
tena na majirani wenye nia ya kuwadhuru
wanaoumiza kama michongoma na miiba
mikali. Ndipo watakapojua kwamba Mimi
ndimi BWANA Mwenyezi.
25 [e]" 'Hili ndilo BWANA Mwenyezi
asemalo: Nitakapoikusanya nyumba
ya Israeli kutoka mataifa ambako
wametawanyika, nitajionyesha kuwa
mtakatifu miongoni mwao machoni
pa mataifa. Ndipo watakapoishi katika
nchi yao wenyewe, niliyompa mtumishi
wangu Yakobo. 26 [f]Wataishi humo kwa
salama na watajenga nyumba na kupanda
mashamba ya mizabibu, wataishi kwa
salama nitakapowaadhibu majirani zao
wote ambao waliwafanyia uovu. Ndipo
watakapojua kwamba Mimi ndimi BWANA,
Mungu wao.' "

*Unabii Dhidi Ya Misri*

29 Katika mwaka wa kumi, mwezi wa
kumi, siku ya kumi na mbili, neno la
BWANA likanijia kusema: 2 [g]"Mwanadamu,
elekeza uso wako juu ya Farao mfalme wa
Misri na utabiri dhidi yake na dhidi ya
Misri yote. 3 [h]Nena, nawe useme: 'Hili ndilo
BWANA Mwenyezi asemalo:

" 'Mimi ni kinyume nawe, Farao, mfalme wa Misri,
joka kubwa ulalaye katikati ya vijito vyako.
Unasema, "Mto Naili ni wangu mwenyewe;
niliufanya kwa ajili yangu mwenyewe."
4 [i]Lakini nitatia ndoana katika mataya yako
nami nitawafanya samaki wa vijito vyako
washikamane na magamba yako.
Nitakutoa katikati ya vijito vyako,
pamoja na samaki wote
walioshikamana na magamba yako.
5 [j]Nitakutupa jangwani,
wewe pamoja na samaki wote wa vijito vyako.
Utaanguka uwanjani,
nawe hutakusanywa au kuchukuliwa.
Nitakutoa uwe chakula
kwa wanyama wa nchi
na ndege wa angani.

6 [k]Ndipo wale wote waishio Misri
watakapojua kuwa Mimi ndimi BWANA.
" 'Umekuwa fimbo ya tete kwa nyumba
ya Israeli. 7 [l]Walipokushika kwa mikono
yao, ulivunjika na kuchana mabega yao;

[a]**28:21** Eze 6:2; 13:17; Yer 25:2; Mwa 10:15
[b]**28:22** Kut 14:4; Za 9:16; Eze 30:19; 39:13; Law 10:3
[c]**28:23** Eze 5:17; 38:22
[d]**28:24** Hes 33:55; Yos 23:13; Isa 5:6; Eze 2:6
[e]**28:25** Za 106:47; Yer 32:37; Isa 11:12; Eze 20:41; Yer 12:15; 12:15; 23:8; Eze 11:17
[f]**28:26** Law 25:18; Yer 23:6; Hos 2:15; Amo 9:14-15; 1Fal 4:25; Yer 17:25; Kum 20:6; Eze 38:8; 39:26-27; Isa 65:21
[g]**29:2** Yer 25:19; Isa 19:1-17; Yer 46:2; Eze 25:2; 30:1-26; 31:1-18
[h]**29:3** Yer 44:30; Za 68:30; Isa 27:1; Eze 32:2; Yer 46:8
[i]**29:4** 2Fal 19:28; Ay 41:2; Eze 38:4
[j]**29:5** Yer 7:33; 34:20; 8:2; Eze 31:13; 32:4-6; 39:4
[k]**29:6** 2Fal 18:21; Isa 36:6
[l]**29:7** Yer 17:5; Eze 17:15-17; 2Fal 18:21; Isa 36:6

walipokuegemea, ulivunjika na migongo
yao ikateguka.
8 [a]“ ‘Kwa hiyo hili ndilo BWANA Mwenyezi
asemalo: Nitaleta upanga juu yako na kuua
watu wako na wanyama wao. 9 [b]Misri
itakuwa ukiwa na isiyolimwa wala kukaliwa
na watu. Ndipo watakapojua kuwa Mimi
ndimi BWANA.
“ ‘Kwa sababu ulisema, “Mto Naili ni
wangu; mimi niliufanya,” 10 [c]kwa hiyo
mimi ni kinyume nawe na kinyume na
vijito vyako, nami nitaifanya nchi ya
Misri kuwa magofu na ukiwa isiyolimwa
wala kukaliwa na watu kuanzia Migdoli
hadi Aswani, hata kufikia mpakani wa
Ethiopia. 11 [d]Hakuna unyayo wa mtu au
mnyama utakaopita ndani yake, wala
hakuna yeyote atakayeishi humo kwa muda
wa miaka arobaini. 12 [e]Nitaifanya nchi ya
Misri ukiwa, miongoni mwa nchi zilizo
ukiwa, nayo miji yake itabaki ukiwa miaka
arobaini miongoni mwa miji iliyo magofu.
Nami nitawatawanya Wamisri miongoni
mwa mataifa na kuwafukuza huku na huko
katika nchi nyingine.
13 [f]“ ‘Lakini hili ndilo BWANA Mwenyezi
asemalo: Mwishoni mwa hiyo miaka
arobaini, nitawakusanya Wamisri kutoka
mataifa walikotawanywa. 14 [g]Nitawarudisha
hao Wamisri kutoka kwenye kutekwa kwao
na kuwaweka katika Pathrosi,[h] nchi ya baba
zao. Huko watakuwa na ufalme usiokuwa
na nguvu. 15 [i]Utakuwa ufalme dhaifu kuliko
zote na kamwe Misri haitajikweza tena juu
ya mataifa mengine. Nitaufanya ufalme
wake dhaifu sana kiasi kwamba kamwe
hautatawala tena juu ya mataifa mengine.
16 [j]Misri haitakuwa tena tumaini la watu
wa Israeli bali itakuwa kumbukumbu
ya dhambi yao kwa kuigeukia kuomba
msaada. Ndipo watakapojua kuwa Mimi
ndimi BWANA Mwenyezi.’ ”
17 [k]Katika mwaka wa ishirini na saba,
mwezi wa kwanza, siku ya kwanza, neno la
BWANA likanijia, kusema: 18 [l]“Mwanadamu,
Nebukadneza mfalme wa Babeli aliongoza
jeshi lake kufanya kazi ngumu dhidi ya
Tiro; kila kichwa kilipata upaa na kila
bega likachunika. Lakini yeye na jeshi
lake hawakupata malipo yoyote kutokana
na muda wote aliongoza hiyo vita dhidi
ya Tiro. 19 [m]Kwa hiyo hili ndilo BWANA
Mwenyezi asemalo: Nitaitia Misri mikononi
mwa Nebukadneza mfalme wa Babeli, naye
atachukua utajiri wa Misri. Atateka mateka
na kuchukua nyara mali za Misri kama ujira
kwa ajili ya jeshi lake. 20 [n]Nimempa mfalme
wa Babeli nchi ya Misri kuwa ujira kwa
juhudi zake kwa sababu yeye na jeshi lake
walifanya kwa ajili yangu, asema BWANA
Mwenyezi.
21 [o]“Katika siku hiyo nitaifanya nyumba
ya Israeli iwe na nguvu nami nitakifungua
kinywa chako miongoni mwao. Ndipo
watakapojua kwamba Mimi ndimi BWANA.”

*Maombolezo Kwa Ajili Ya Misri*

30 Neno la BWANA likanijia kusema:
2 [p]“Mwanadamu, toa unabii na useme:
‘Hili ndilo BWANA Mwenyezi asemalo:

“ ‘Ombolezeni ninyi na mseme,
“Ole wa siku ile!”
3 [q]Kwa kuwa siku ile imekaribia,
siku ya BWANA imekaribia,
siku ya mawingu,
siku ya maangamizi kwa mataifa.

[a]**29:8** Eze 14:17; 25:13; 32:11-13
[b]**29:9** Eze 30:7-8, 13-19; Mit 16:18; Yer 46:8
[c]**29:10** Eze 30:6-12; Yer 21:13; Kut 3:22; Yer 46:19; Kut 14:2; Isa 18:1
[d]**29:11** Eze 32:13
[e]**29:12** Yer 46:19; Eze 30:7; 34:10
[f]**29:13** Isa 19:23; Yer 46:26
[g]**29:14** Isa 11:11; Eze 30:14; 17:14; Isa 19:22; Yer 46:26
[h]14 Pathrosi ni Misri ya Juu.
[i]**29:15** Zek 10:11
[j]**29:16** 2Nya 32:10; Isa 20:5; Hos 8:13; Isa 30:2; Mao 4:17; Hes 5:15
[k]**29:17** Eze 30:20; 24:1; 40:1
[l]**29:18** Yer 27:6; Law 13:40; Ay 1:20; Yer 39:1
[m]**29:19** Yer 43:10-13; Eze 32:11; Yer 27:6; Isa 19:4; Eze 26:5; 30:4, 10
[n]**29:20** Isa 45:1; Yer 25; 9; Isa 43:3; 10:6-7
[o]**29:21** Lk 1:69; 1Sam 2:10; Za 132:17; Eze 33:22; 3:27; 24:27
[p]**30:2** Isa 13:6; Yak 5:1
[q]**30:3** Oba 1:15; Yoe 2:11; Eze 32:7; 34:12; 7:7; Yoe 1:15

4 [a]Upanga utakuja dhidi ya Misri,
nayo maumivu makuu yataijia
Ethiopia.
Mauaji yatakapoangukia Misri,
utajiri wake utachukuliwa
na misingi yake itabomolewa.

5 [b]Kushi[c] na Putu, Ludi na Arabia yote,
Libya[d] na watu wa nchi ya Agano watauawa
kwa upanga pamoja na Misri.
6 [e]“ ‘Hili ndilo BWANA asemalo:

“ ‘Wale walioungana na Misri
wataanguka
na kiburi cha nguvu zake
kitashindwa.
Kutoka Migdoli hadi Aswani,
watauawa ndani yake kwa
upanga,
asema BWANA Mwenyezi.

7 [f]“ ‘Hizo nchi zitakua ukiwa
miongoni mwa nchi zilizo ukiwa,
nayo miji yao itakuwa magofu
miongoni mwa miji iliyo magofu.
8 [g]Ndipo watakapojua kwamba mimi
ndimi BWANA,
nitakapoiwasha Misri moto
na wote wamsaidiao watapondwa.

9 [hi]“ ‘Siku hiyo wajumbe watatoka
kwangu kwa merikebu, ili kuwatia hofu
Ethiopia, wakiwa katika hali yao ya
kuridhika. Maumivu makali yatawapata
siku ya maangamizi ya Misri, kwa kuwa
hakika itakuja.
10 [j]“ ‘Hili ndilo BWANA Mwenyezi
asemalo:

“ ‘Nitakomesha makundi ya wajeuri
ya Misri
kwa mkono wa Nebukadneza
mfalme wa Babeli.
11 [k]Yeye na jeshi lake, taifa lililo katili
kuliko mataifa yote,
litaletwa ili kuangamiza nchi.
Watafuta panga zao dhidi ya Misri
na kuijaza nchi kwa waliouawa.
12 [l]Nitakausha vijito vya Naili
na nitaiuza nchi kwa watu waovu,
kwa mkono wa wageni,
nitaifanya nchi ukiwa na kila kitu
kilichomo ndani yake.

Mimi BWANA nimenena haya.

13 [m]“ ‘Hili ndilo BWANA Mwenyezi
asemalo:

“ ‘Nitaangamiza sanamu
na kukomesha vinyago katika
Memfisi[n]
Hapatakuwepo tena na mkuu katika
nchi ya Misri,
nami nitaeneza hofu katika nchi
nzima.
14 [o]Nitaifanya Pathrosi[p] kuwa ukiwa
na kuitia moto Soani,
nami nitaipiga kwa adhabu
Thebesi[q]
15 Nitaimwaga ghadhabu yangu juu ya
Pelusiumu,[r]
ngome ya Misri,
nami nitakatilia mbali
makundi ya wajeuri wa Thebesi.
16 [s]Nitaitia moto nchi ya Misri;
Pelusiumu itagaagaa kwa
maumivu makuu.

---

[a]**30:4** Eze 29:19; Yer 50:15; 25:19; Dan 11:43; Mwa 10:6; Eze 29:10
[b]**30:5** Eze 27:10; Yer 25:20; 2Nya 9:14; Nah 3:9
[c]5 Kushi ndiyo Ethiopia.
[d]5 Libya ndiyo Kubu.
[e]**30:6** Eze 29:10
[f]**30:7** Eze 29:12
[g]**30:8** Yer 49:27; Eze 39:6; Nah 1:6; Eze 29:9
[h]**30:9** Kum 31:6; Mt 10:28; Eze 24:3; 44:6
[i]**30:9** Mwa 10:6; Isa 18:1-2; 23:5; Eze 32:9-10; Sef 2:12
[j]**30:10** Yer 39:1; Eze 29:19
[k]**30:11** Eze 28:7; 29:19
[l]**30:12** Isa 19:6; Yer 46:8; Eze 29:9; 19:7
[m]**30:13** Yer 43:12; Isa 19:13; Eze 6:6; Zek 10:11
[n]13 Kiebrania ni Nofu.
[o]**30:14** Eze 29:14; Hes 13:22; Za 78:12; Yer 46:25
[p]14 Pathrosi ni Misri ya Juu.
[q]14 Thebesi kwa Kiebrania ni No (au No-Amoni), mji katika Misri.
[r]15 Kiebrania ni Sini.
[s]**30:16** Yos 7:15; Isa 19:13

Thebesi itachukuliwa na tufani,
Memfisi itakuwa katika taabu daima.
17 [a]Wanaume vijana wa Oni[b] na wa Pi-Besethi[c]
wataanguka kwa upanga
nayo hiyo miji itatekwa.
18 [d]Huko Tahpanhesi mchana utatiwa giza
nitakapovunja kongwa la Misri;
hapo kiburi cha nguvu zake kitakoma.
Atafunikwa na mawingu
na vijiji vyake vitatekwa.
19 [e]Kwa hiyo nitaipiga Misri kwa adhabu,
nao watajua kuwa Mimi ndimi BWANA.' "

20 [f]Katika mwaka wa kumi na moja,
mwezi wa kwanza, siku ya saba, neno la
BWANA likanijia kusema: 21 [g]"Mwanadamu,
nimevunja mkono wa Farao mfalme wa
Misri. Haukufungwa ili upone au kuwekewa
kipande cha ubao ili upate nguvu za
kuweza kuchukua upanga. 22 [h]Kwa hiyo
hili ndilo BWANA Mwenyezi asemalo: Mimi
ni kinyume na Farao mfalme wa Misri.
Nitavunja mikono yake yote miwili, ule
mkono ulio mzima pia na ule uliovunjika
na kuufanya upanga uanguke toka mkononi
mwake. 23 [i]Nitawatawanya Wamisri
miongoni mwa mataifa na kuwafukuza
huku na huko katika nchi zote. 24 [j]Nitaitia
nguvu mikono ya mfalme wa Babeli na
kuutia upanga wangu mkononi mwake,
lakini nitavunja mikono ya Farao, naye
atalia kwa huzuni mbele yake kama mtu
aliyetiwa jeraha la kumfisha. 25 [k]Nitaitia
nguvu mikono ya mfalme wa Babeli,
lakini mikono ya Farao italegea. Ndipo
watakapojua kwamba Mimi ndimi BWANA,
nitakapoutia upanga wangu mkononi mwa
mfalme wa Babeli, naye ataunyoosha dhidi
ya Misri. 26 [l]Nitawatawanya Wamisri
miongoni mwa mataifa na kuwafukuza
huku na huko katika nchi mbalimbali.
Ndipo watakapojua kwamba Mimi ndimi
BWANA."

### *Mwerezi Katika Lebanoni*

31 [m]Katika mwaka wa kumi na moja,
mwezi wa tatu, siku ya kwanza, neno la
BWANA likanijia, kusema: 2 [n]"Mwanadamu,
mwambie Farao mfalme wa Misri na
makundi yake ya wajeuri:

" 'Je, ni nani awezaye kulinganishwa
na wewe katika fahari.
3 [o]Angalia Ashuru, wakati fulani ilikuwa mwerezi huko Lebanoni,
ukiwa na matawi mazuri ukitia msitu kivuli;
ulikuwa mrefu sana,
kilele chake kilipita majani ya miti yote.
4 [p]Maji mengi yaliustawisha,
chemchemi zenye maji mengi ziliufanya urefuke;
vijito vyake vilitiririka pale
ulipoota pande zote
na kupeleka mifereji yake
kwenye miti yote ya shambani.
5 [q]Hivyo ukarefuka
kupita miti yote ya shambani;

---

[a]**30:17** Mwa 41:45
[b]17 Yaani Heliopoli (Mji wa Jua).
[c]17 Yaani Bubasti.
[d]**30:18** Law 26:13; Isa 9:4; Yer 2:16; 43:7
[e]**30:19** Eze 28:22
[f]**30:20** Eze 26:1; 29:17; 32:1
[g]**30:21** Yer 48:25; 44:30; 30:13; 46:11
[h]**30:22** Mwa 15:18; Yer 46:25; Za 37:17; Zek 11:17
[i]**30:23** Eze 29:12
[j]**30:24** Zek 10:6-12; 12:5; Eze 21:14; Sef 2:12; Yer 51:52
[k]**30:25** Kut 7:5; Za 9:16; 59:13; 1Nya 21:12; Isa 10:5; Eze 29:19
[l]**30:26** Eze 29:12
[m]**31:1** Yer 52:5; Eze 32:17; 30:20
[n]**31:2** Eze 31:18
[o]**31:3** Nah 3:18; Isa 10:34; Eze 19:11; Sef 2:13; Yer 50:18; 2Fal 19:23; Hab 2:17; Zek 11:1
[p]**31:4** Eze 17:7; Dan 4:10
[q]**31:5** Hes 24:6; Eze 17:5; Dan 4:11

vitawi vyake viliongezeka
na matawi yake yakawa marefu,
yakitanda kwa sababu ya wingi
wa maji.
6 [a]Ndege wote wa angani
wakaweka viota kwenye vitawi
vyake,
wanyama wote wa shambani
wakazaana chini ya matawi yake,
mataifa makubwa yote
yaliishi chini ya kivuli chake.
7 [b]Ulikuwa na fahari katika uzuri,
ukiwa na matawi yaliyotanda,
kwa kuwa mizizi yake ilikwenda
chini
mpaka kwenye maji mengi.
8 [c]Mierezi katika bustani ya Mungu
haikuweza kushindana nao,
wala misunobari haikuweza
kulingana na vitawi vyake,
wala miaramoni
haikulinganishwa na matawi yake,
wala hakukuwa na mti katika
bustani ya Mungu
wa kulinganisha na uzuri wake.
9 [d]Niliufanya kuwa mzuri
ukiwa na matawi mengi,
ulionewa wivu na miti yote ya Edeni
katika bustani ya Mungu.

10 [e]" 'Kwa hiyo hili ndilo BWANA
Mwenyezi asemalo: Kwa sababu ulikuwa
mrefu sana, kilele chake kikiwa juu ya
majani manene ya miti na kwa sababu
ulikuwa na kiburi cha urefu wake,
11 [f]niliutia
mikononi mwa mtawala wa mataifa, ili
yeye aushughulikie sawasawa na uovu
wake. Nikaukatilia mbali,
12 [g]nayo mataifa
mageni yaliyo makatili sana yaliukata huo
mti na kuuacha. Matawi yake yalianguka
juu ya milima na kwenye mabonde yote,
vitawi vyake vikavunjika na kusambaa
katika makorongo yote ya nchi. Mataifa
yote ya duniani yakaondoka kutoka kwenye
kivuli chake na kuuacha.
13 [hi]Ndege wote wa
angani wakakaa kwenye ule mti ulioanguka
na wanyama pori wote wakakaa katikati
ya vitawi vyake.
14 [j]Kamwe hakutakuwa
na miti mingine kando ya hayo maji
itakayorefuka zaidi ya huo, vilele vyake
vikiwa juu ya majani yote ya miti. Hakuna
miti mingine, hata kama imekunywa maji
vizuri namna gani, itakayofikia urefu huo.
Yote mwisho wake ni kifo, na kuingia
ardhini, kama vile ilivyo kwa wanadamu,
pamoja na wale waendao shimoni.

15 [k]" 'Hili ndilo BWANA Mwenyezi asemalo:
Katika siku ile mwerezi uliposhushwa chini
kaburini[l] nilizifunika chemchemi zenye maji
mengi kwa maombolezo: Nilivizuia vijito
vyake na wingi wa maji yake nikauzuia.
Kwa sababu yake niliivika Lebanoni huzuni,
nayo miti yote ya shambani ikanyauka.
16 [m]Niliyafanya mataifa yatetemeke kwa
kishindo cha kuanguka kwake wakati
nilipoushusha chini kaburini pamoja na
wale washukao shimoni. Ndipo miti yote
ya Edeni, miti iliyo bora kuliko yote na
iliyo mizuri sana ya Lebanoni, miti yote
ile iliyokunywa maji vizuri, ilifarijika
hapa duniani.
17 [n]Wale walioishi katika
kivuli chake, wale walioungana naye
miongoni mwa mataifa, nao pia walikuwa
wamezikwa pamoja naye, wakiungana na
wale waliouawa kwa upanga.

18 [o]" 'Ni miti ipi ya Edeni inayoweza
kulinganishwa nawe kwa fahari na utukufu?
Hata hivyo, wewe pia, utashushwa chini
pamoja na miti ya Edeni mpaka kuzimu,

---

[a]**31:6** Eze 17:23; Mt 13:32; Dan 4:12; Mwa 31:7-9
[b]**31:7** Ay 14:9
[c]**31:8** Za 80:10; Mwa 2:8-9; 30:37
[d]**31:9** Kut 9:16; Dan 4:22-24; Mwa 13:10; Eze 28:13
[e]**31:10** Isa 2:11; 14:13-14; Ay 40:11-12; Mit 16:18; Dan 5:20; Eze 28:17
[f]**31:11** Dan 5:20
[g]**31:12** Eze 32:5; 28:7; 32:11-12; 35:8; Dan 4:12-14
[h]**31:13** Isa 18:6; Eze 29:5; 32:4
[i]**31:13** Isa 18:6; Eze 29:5; 32:4
[j]**31:14** Za 82:7; Hes 14:11; Za 63:9; Eze 32:18; Za 49:14
[k]**31:15** 2Sam 1:21
[l]15 Yaani Kuzimu, Sheol kwa Kiebrania; pia mstari 16, 17.
[m]**31:16** Yer 49:21; Eze 26:15; Isa 14:8; Eze 32:18, 31; Isa 14:15; Eze 14:22
[n]**31:17** Za 9:17
[o]**31:18** Yer 9:26; Eze 32:19-21; 28:10

utalala miongoni mwa wasiotahiriwa, pamoja na wale waliouawa kwa upanga.

" 'Huyu ni Farao pamoja na makundi yake yote ya wajeuri, asema BWANA Mwenyezi.' "

*Maombolezo Kwa Ajili Ya Farao*

32 [a]Katika mwaka wa kumi na mbili,
mwezi wa kumi na mbili, siku
ya kwanza ya mwezi, neno la BWANA
likanijia, kusema: 2 [b]"Mwanadamu, fanya
maombolezo kwa ajili ya Farao mfalme wa
Misri na umwambie:

" 'Wewe ni kama simba miongoni
mwa mataifa,
wewe ni kama joka kubwa
baharini,
unayevuruga maji kwa miguu yako
na kuchafua vijito.

3 [c]" 'Hili ndilo BWANA Mwenyezi asemalo:

" 'Nikiwa pamoja na wingi mkubwa
wa watu
nitautupa wavu wangu juu yako,
nao watakukokota katika wavu
wangu.
4 [d]Nitakutupa nchi kavu
na kukuvurumisha uwanjani.
Nitawafanya ndege wote wa angani
watue juu yako
na wanyama wote wa nchi
watajishibisha nyama yako.
5 [e]Nitatawanya nyama yako juu ya
milima
na kujaza mabonde kwa mabaki
yako.
6 [f]Nitailowanisha nchi kwa damu yako
inayotiririka
njia yote hadi milimani,
nayo mabonde yatajazwa na
nyama yako.
7 [g]Nitakapokuzimisha, nitafunika
mbingu
na kuzitia nyota zake giza;
nitalifunika jua kwa wingu,
nao mwezi hautatoa nuru yake.
8 [h]Mianga yote itoayo nuru angani
nitaitia giza juu yako;
nitaleta giza juu ya nchi yako,
asema BWANA Mwenyezi.
9 Nitaifadhaisha mioyo ya mataifa
mengi
nitakapokuangamiza miongoni
mwa mataifa,
nikikuleta uhamishoni miongoni
mwa nchi
ambazo haujapata kuzijua.
10 [i]Nitayafanya mataifa mengi
wakustaajabie,
wafalme wao watatetemeka
kwa hofu kwa ajili yako
nitakapotikisa upanga wangu
mbele yao.
Siku ya anguko lako
kila mmoja wao atatetemeka
kila dakika kwa ajili ya maisha
yake.

11 [j]" 'Kwa kuwa hili ndilo BWANA
Mwenyezi asemalo:

" 'Upanga wa mfalme wa Babeli
utakuja dhidi yako.
12 [k]Nitafanya makundi yako ya wajeuri
kuanguka
kwa panga za watu mashujaa,
taifa katili kuliko mataifa yote.
Watakivunjavunja kiburi cha Misri,
nayo makundi yake yote
ya wajeuri yatashindwa.
13 [l]Nitaangamiza mifugo yake yote
wanaojilisha kando ya maji mengi,

---

[a]**32:1** Eze 31:1; 33:21
[b]**32:2** 2Sam 1:17; 2Nya 35:25; 2Fal 24:1; Nah 2:11-13; Ay 41:31; Eze 29:3; Ay 3:8; Eze 34:18; 2Sam 3:33
[c]**32:3** Eze 12:13; Hab 1:15
[d]**32:4** Isa 18:6; 1Sam 17:44-46; Eze 39:4-5; 31:12-13
[e]**32:5** Eze 31:12
[f]**32:6** Isa 34:3; Eze 29:5
[g]**32:7** Yoe 3:15; Mt 24:29; Ufu 6:12; Isa 34:4; Eze 30:3; Yoe 2:2
[h]**32:8** Za 102:26; Ay 9:7; Yer 4:23; Yoe 2:10
[i]**32:10** Yer 46:10; Eze 26:16; Ufu 18:9-10; Isa 30:32; Eze 27:35; 30:9
[j]**32:11** Isa 19:4; Yer 46:26; Eze 21:19; 46:13; 29:19
[k]**32:12** Eze 28:7; 31:11-12
[l]**32:13** Eze 29:8-11

hayatavurugwa tena kwa mguu wa
mwanadamu
wala kwato za mnyama
hazitayachafua tena.
14 Kisha nitafanya maji yake yatulie
na kufanya vijito vyake
vitiririke kama mafuta,
asema BWANA Mwenyezi.
15 [a]Nitakapoifanya Misri kuwa ukiwa
na kuiondolea nchi kila kitu
kilichomo ndani yake,
nitakapowapiga wote waishio humo,
ndipo watakapojua kuwa
Mimi ndimi BWANA.'

16 [b]"Hili ndilo ombolezo watakalomwimbia.
Binti za mataifa wataliimba, kwa kuwa
Misri na makundi yake yote ya wajeuri
wataliimba, asema BWANA Mwenyezi."

17 Katika mwaka wa kumi na mbili,
mwezi wa kwanza, siku ya kumi na
tano ya mwezi, neno la BWANA likanijia
kusema:
18 [c]"Mwanadamu, omboleza
kwa ajili ya makundi ya wajeuri wa
Misri na uwatupe kuzimu yeye na binti
za mataifa yenye nguvu, waende huko
pamoja nao washukao shimoni.
19 [d]Je,
ninyi mnamzidi nani kwa uzuri? Shukeni
chini! Nanyi mkalazwe pamoja na hao
wasiotahiriwa!
20 [e]Wataanguka miongoni
mwa wale waliouawa kwa upanga. Upanga
umefutwa, mwache aburutwe mbali pamoja
na hao wajeuri wake wote.
21 [f]Kutoka
kuzimu viongozi hodari watanena kuhusu
Misri pamoja na wale walioungana nao,
'Wameshuka chini, nao wamelala kimya
pamoja na hao wasiotahiriwa, pamoja na
wale waliouawa kwa upanga.'
22 [g]"Ashuru yuko huko pamoja na jeshi
lake lote, amezungukwa na makaburi ya
watu wake wote waliouawa, wale wote
walioanguka kwa upanga.
23 [h]Makaburi
yao yako kwenye kina cha chini cha shimo
na jeshi lake limelala kulizunguka kaburi
lake. Wote waliokuwa wameeneza hofu
kuu katika nchi ya walio hai wameuawa,
wameanguka kwa upanga.
24 [i]"Elamu yuko huko, pamoja na
makundi yake yote ya wajeuri wakiwa
wamelizunguka kaburi lake. Wote
wameuawa, wameanguka kwa upanga.
Wote waliokuwa wameeneza hofu katika
nchi ya walio hai walishuka kuzimu bila
kutahiriwa. Wanaichukua aibu yao pamoja
na wale washukao shimoni.
25 [j]Kitanda
kimetandikwa kwa ajili yake miongoni
mwa waliouawa, pamoja na makundi yake
yote ya wajeuri wakiwa wamelizunguka
kaburi lake. Wote ni watu wasiotahiriwa,
wameuawa kwa upanga. Kwa sababu
vitisho vyao vilienea katika nchi ya walio
hai, wameichukua aibu yao pamoja na
wale washukao shimoni, nao wamewekwa
miongoni mwa waliouawa.
26 [k]"Mesheki na Tubali wako humo,
pamoja na makundi yao ya wajeuri
wakiwa wameyazunguka makaburi yao.
Wote hawakutahiriwa, wameuawa kwa
upanga kwa sababu walieneza vitisho vyao
katika nchi ya walio hai.
27 Je, hawakulala
na mashujaa wengine wasiotahiriwa
waliouawa, ambao wameshuka kaburini
wakiwa na silaha zao za vita, ambao panga
zao ziliwekwa chini ya vichwa vyao na
uovu wao juu ya mifupa yao? Adhabu kwa
ajili ya dhambi zao ilikuwa juu ya mifupa
yao, ingawa vitisho vya mashujaa hawa
vilikuwa vimeenea hadi kwenye nchi ya
walio hai.
28 "Wewe pia, ee Farao, utavunjwa nawe
utalala miongoni mwa wasiotahiriwa,
pamoja na wale waliouawa kwa upanga.
29 [l]"Edomu yuko humo, wafalme wake
wote na wakuu wake wote, ambao

[a]**32:15** Kut 7:5; Za 107:33-34; Kut 14:4; 18
[b]**32:16** Mwa 50:10; 2Sam 1:17; Eze 26:17; 19:1
[c]**32:18** Yer 1:10; Mik 1:8; Eze 26:20; 31:14-16; 32:1
[d]**32:19** Eze 28:10; 31:18
[e]**32:20** Za 28:3; Eze 31:17-18
[f]**32:21** Isa 14:9; Eze 28:10
[g]**32:22** Eze 32:24, 26, 29, 30
[h]**32:23** Isa 14:15; Nah 1:14
[i]**32:24** Mwa 10:22; Yer 49:37; Ay 28:13; Eze 26:20
[j]**32:25** Eze 28:10; 28:10
[k]**32:26** Mwa 10:2; Eze 27:13
[l]**32:29** Za 137:7; Eze 25:12-14; 35:15; Yer 49:7; Isa 34:5-15

ijapokuwa wana nguvu, wamelazwa pamoja
na wale waliouawa kwa upanga. Wamelala
pamoja na wasiotahiriwa, pamoja na wale
washukao shimoni.
30 [a]“Wakuu wote wa kaskazini na
Wasidoni wote wako huko, wameshuka
chini pamoja na waliouawa kwa aibu
ijapokuwa kuna vitisho vilivyosababishwa
na nguvu zao. Wamelala bila kutahiriwa
pamoja na wale waliouawa kwa upanga
na kuchukua aibu yao pamoja na wale
washukao chini shimoni.
31 [b]“Farao, yeye pamoja na jeshi lake
lote, atakapowaona atafarijiwa kwa ajili
ya makundi yake yote ya wajeuri, wale
waliouawa kwa upanga, asema Bwana
Mwenyezi. 32 [c]Ingawa nilimfanya Farao
aeneze vitisho vyake katika nchi ya walio
hai, Farao pamoja na makundi yake yote
ya wajeuri watalazwa miongoni mwa
wasiotahiriwa, pamoja na wale waliouawa
kwa upanga, asema Bwana Mwenyezi.”

### *Wajibu Wa Ezekieli Kuwa Mlinzi Kwa Watu Wake*

33 Neno la Bwana likanijia kusema:
2 [d]“Mwanadamu, sema na watu wako
uwaambie, ‘Nitakapoleta upanga dhidi
ya nchi, nao watu wa nchi wakamchagua
mmoja wa watu wao na kumfanya awe
mlinzi wao, 3 [e]naye auonapo upanga
unakuja dhidi ya nchi na kupiga tarumbeta
kuonya watu, 4 [f]kama mtu yeyote asikiapo
sauti ya tarumbeta hakukubali kuonywa,
basi upanga ujapo na kuutoa uhai wake,
damu yake itakuwa juu ya kichwa chake
mwenyewe. 5 [g]Kwa kuwa alisikia sauti
ya tarumbeta lakini hakukubali maonyo,
damu yake itakuwa juu ya kichwa chake
mwenyewe. Kama angekubali maonyo,
angelijiokoa mwenyewe. 6 [h]Lakini kama
mlinzi akiona upanga unakuja na asipige
tarumbeta kuonya watu na upanga ukija
na kutoa uhai wa mmoja wao, yule mtu
ataondolewa kwa sababu ya dhambi yake,
lakini damu yake nitaitaka mkononi mwa
mlinzi huyo.’
7 [i]“Mwanadamu, nimekufanya wewe
kuwa mlinzi kwa ajili ya nyumba ya Israeli,
kwa hiyo sikia neno nisemalo na uwape
maonyo kutoka kwangu. 8 [j]Nimwambiapo
mtu mwovu, ‘Ewe mtu mwovu, hakika
utakufa,’ nawe hukusema neno la
kumwonya ili atoke katika njia zake, yule
mtu mwovu atakufa kwa ajili ya dhambi
yake, mimi nitaitaka damu yake mkononi
mwako. 9 [k]Lakini kama utamwonya huyo
mtu mwovu aache njia zake mbaya naye
hafanyi hivyo, atakufa kwa ajili ya dhambi
yake, lakini utakuwa umejiokoa mwenyewe.
10 [l]“Mwanadamu, sema na nyumba ya
Israeli uwaambie, ‘Hili ndilo mnalosema:
“Makosa yetu na dhambi zetu zimetulemea,
nasi tunadhoofika kwa sababu ya hayo.
Tutawezaje basi kuishi?” ’ 11 [m]Waambie,
‘Hakika kama mimi niishivyo, asema
Bwana Mwenyezi, sifurahii kifo cha watu
waovu, bali kwamba wageuke kutoka
njia zao mbaya wapate kuishi. Geukeni!
Geukeni kutoka njia zenu mbaya! Kwa nini
mkafe, ee nyumba ya Israeli?’
12 [n]“Kwa hiyo, mwanadamu, waambie
watu wako, ‘Haki ya mtu mwenye haki
haitamwokoa wakati anapoacha kutii, wala
uovu wa mtu mwovu hautamsababisha
yeye kuanguka anapotubu na kuacha uovu.
Mtu mwenye haki, kama akitenda dhambi,
hataishi kwa sababu ya uadilifu wake
wa awali.’ 13 [o]Kama nikimwambia mtu

[a]**32:30** Isa 14:31; Yer 25:26; Mwa 10:15; Eze 38:6; Yer 25:22; Eze 28:10; 28:8
[b]**32:31** Eze 14:22; 31:16
[c]**32:32** Yer 44:30; Ay 3:14
[d]**33:2** Law 26:25; Yer 12:12; Isa 14:16; 21:6-9; Yer 51:12
[e]**33:3** Hes 10:7; Hos 5:8; Kut 20:18
[f]**33:4** 2Nya 25:16; Mdo 18:6; Eze 18:13; Law 20:9; Yer 6:17
[g]**33:5** Law 20:9; Kut 9:21
[h]**33:6** Isa 56:10-11; Eze 3:18
[i]**33:7** Isa 52:8; Yer 26:5
[j]**33:8** Eze 33:14; Isa 3:11; Eze 18:14
[k]**33:9** Eze 3:17-19; Mdo 13:46; Lk 12:4; Za 7:12
[l]**33:10** Law 26:16; Eze 24:23; 4:17
[m]**33:11** 2Sam 14:14; Mao 3:33; 2Pet 3:9; Yoe 2:12; 1Tim 2:4; 2Nya 30:9; Yer 3:12; Isa 19:22; Yer 44:7-8
[n]**33:12** 2Nya 7:14; Eze 18:21; 3:20
[o]**33:13** Eze 18:23; Ebr 10:38; Lk 18:9; 2Pet 2:20-21

mwenye haki kwamba hakika utaishi, lakini
akategemea hiyo haki yake na kutenda
uovu, hakuna tendo lolote la haki alilotenda
litakalokumbukwa, atakufa kwa ajili ya uovu
alioutenda. 14 [a]Nami kama nikimwambia
mtu mwovu, ‘Hakika utakufa,’ kisha
akageuka kutoka dhambi yake na kufanya
lile lililo haki na sawa, 15 [b]kama akirudisha
kile alichochukua rehani kwa ajili ya deni,
akarudisha alichoiba na kufuata amri zile
ziletazo uzima, wala hafanyi uovu, hakika
ataishi, hatakufa. 16 [c]Hakuna dhambi yoyote
aliyoitenda itakayokumbukwa juu yake.
Ametenda lile lililo haki na sawa, hakika
ataishi.

17 [d]“Lakini watu wako wanasema, ‘Njia ya
Bwana si sawa.’ Lakini ni njia zao ambazo si
sawa. 18 [e]Kama mtu mwenye haki akigeuka
kutoka uadilifu wake na kufanya uovu,
atakufa kwa ajili ya huo uovu. 19 [f]Naye
mtu mwovu kama akigeuka kutoka uovu
wake na kufanya lile lililo haki na sawa,
kwa kufanya hivyo ataishi. 20 [g]Lakini, ee
nyumba ya Israeli, unasema, ‘Njia ya Bwana
si sawa.’ Lakini nitamhukumu kila mmoja
wenu sawasawa na njia zake mwenyewe.”

*Anguko La Yerusalemu Laelezewa*

21 [h]Mwaka wa kumi na mbili wa uhamisho
wetu, mwezi wa kumi, siku ya tano, mtu
aliyekuwa ametoroka kutoka Yerusalemu
akanijia na kusema, “Mji wa Yerusalemu
umeanguka!” 22 [i]Basi jioni kabla mtu huyo
hajaja, mkono wa Bwana, ulikuwa juu
yangu, naye alifungua kinywa changu kabla
ya mtu yule aliyenijia asubuhi hajafika. Basi
kinywa changu kilifunguliwa na sikuweza
tena kunyamaza.

23 Ndipo neno la Bwana likanijia
kusema: 24 [j]“Mwanadamu, watu wanaoishi
katika magofu hayo katika nchi ya Israeli
wanasema hivi, ‘Abrahamu alikuwa mtu
mmoja tu, hata hivyo akaimiliki nchi.
Lakini sisi ni wengi, hakika tumepewa nchi
kuwa milki yetu.’ 25 [k]Kwa hiyo waambie,
‘Hili ndilo Bwana Mwenyezi asemalo:
Kwa kuwa mnakula nyama pamoja na
damu na kuinulia sanamu zenu macho
na kumwaga damu, je, mtaimiliki nchi?
26 [l]Mnategemea panga zenu, mnafanya
mambo ya machukizo na kila mmoja
wenu humtia unajisi mke wa jirani yake.
Je, mtaimiliki nchi?’

27 [m]“Waambie hivi: ‘Hili ndilo Bwana
Mwenyezi asemalo: Hakika kama niishivyo,
wale waliobaki katika magofu wataanguka
kwa upanga, wale walio nje mashambani
nitawatoa wararuliwe na wanyama pori,
nao wale walio katika ngome na kwenye
mapango watakufa kwa tauni. 28 [n]Nitaifanya
nchi kuwa ukiwa na utupu na kiburi cha
nguvu zake zitafikia mwisho, nayo milima
ya Israeli itakuwa ukiwa ili mtu yeyote
asipite huko. 29 [o]Kisha watajua kuwa Mimi
ndimi Bwana, nitakapokuwa nimeifanya
nchi kuwa ukiwa na utupu kwa sababu ya
mambo yote ya machukizo waliyotenda.’

30 [p]“Kwa habari yako wewe, mwanadamu,
watu wako wanaongea habari zako wakiwa
karibu na kuta na kwenye milango ya
nyumba, wakiambiana kila mmoja na
mwenzake, ‘Njooni msikie ujumbe ule
utokao kwa Bwana.’ 31 [q]Watu wangu
wanakujia, kama wafanyavyo, nao wanaketi
mbele yako kama watu wangu na kusikiliza
maneno yako, lakini hawayatendi. Kwa
maana udanganyifu u katika midomo yao,

[a]**33:14** Yer 22:3; Eze 18:27
[b]**33:15** Kut 22:1-4; Law 6:2-5; Lk 19:8; Isa 55:7; Yer 18:7-8
[c]**33:16** Isa 43:25; Eze 18:22-26; Yer 50:20
[d]**33:17** Eze 33:20; 18:25-29
[e]**33:18** Eze 3:20; 18:26; Yer 18:10
[f]**33:19** Eze 33:14-15
[g]**33:20** Ay 34:11; Eze 33:17; 18:25-29
[h]**33:21** Eze 24:26; 2Fal 25:4, 10; Yer 52:4-7; Eze 32:1
[i]**33:22** Eze 3:26-27; 24:27; Lk 1:64; Eze 29:21
[j]**33:24** Eze 36:4; Isa 51:2; Lk 3:8; Mik 3:11; Mdo 7:5; Yer 40:7; Eze 11:15
[k]**33:25** Mwa 9:4; Kum 12:16; Yer 7:9-10; Eze 22:6, 27; Yer 7:21
[l]**33:26** Yer 41:7; Eze 22:11
[m]**33:27** 1Sam 13:6; Isa 2:19; Amu 6:2; Yer 42:22; Eze 7:15; 14:21
[n]**33:28** Isa 41:15; Mwa 6:7; Yer 9:10
[o]**33:29** Law 26:34; Yer 18:16; 44:22; Eze 36:4; Mik 7:13
[p]**33:30** Isa 29:13
[q]**33:31** Eze 8:1; Isa 33:15; Mt 13:22; Za 119:36; 78:36-37; Isa 29:13; Yer 3:10

lakini mioyo yao ina tamaa ya faida isiyo halali. 32 [a]Naam, mbele yao umekuwa tu kama yeye aimbaye nyimbo za mapenzi kwa sauti nzuri za kuvutia na kupiga vyombo kwa ustadi, kwa kuwa wanasikia maneno yako lakini hawayatendi.

33 [b]"Wakati mambo haya yote yatakapotimia, kwa kuwa hakika yatatokea, ndipo watakapojua kwamba nabii amekuwepo miongoni mwao."

*Wachungaji Na Kondoo*

34 Neno la BWANA likanijia kusema: 2 [c]"Mwanadamu, tabiri juu ya wachungaji wa Israeli, tabiri na uwaambie: 'Hili ndilo BWANA Mwenyezi asemalo: Ole wa wachungaji wa Israeli ambao hujitunza wenyewe tu! Je, haiwapasi wachungaji kutunza kundi la kondoo? 3 [d]Mnakula mafuta ya wanyama, mnavaa mavazi ya sufu na kuchinja kondoo walionona, lakini hamlitunzi kundi. 4 [e]Hamkuwatia nguvu walio dhaifu wala hamkuwaganga wenye maradhi wala kuwafunga waliojeruhiwa. Hamkuwarudisha waliotangatanga wala kuwatafuta wale waliopotea. Badala yake mmewatawala kwa ukali na kwa ukatili. 5 [f]Hivyo walitawanyika kwa sababu hapakuwepo mchungaji, nao walipotawanyika, wakawa chakula cha wanyama wa mwitu wote. 6 [g]Kondoo wangu walitawanyika, wakatangatanga kwenye milima yote na kwenye kila kilima kirefu. Kondoo wangu walitawanyika juu ya uso wa dunia yote bila kuwa na yeyote wa kuwaulizia wala wa kuwatafuta.

7 " 'Kwa hiyo, ninyi wachungaji, lisikieni neno la BWANA: 8 [h]Kwa hakika kama niishivyo, asema BWANA Mwenyezi, kwa sababu kondoo zangu wamekosa mchungaji na hivyo wametekwa nyara na kuwa chakula cha wanyama wote wa mwituni na kwa sababu wachungaji wangu, hawakuwatafuta kondoo zangu, bali wachungaji wamejitunza wenyewe, nao hawakuwalisha kondoo zangu, 9 [i]kwa hiyo enyi wachungaji, sikieni neno la BWANA: 10 [j]Hili ndilo BWANA Mwenyezi asemalo: Mimi ni kinyume na wachungaji nami nitawadai kondoo zangu mikononi mwao. Nitawafukuza kutoka kwenye kuchunga kundi langu, ili wachungaji wasiendelee kujitunza wenyewe. Nitaokoa kondoo zangu kutoka kwenye vinywa vyao, nao kondoo hawatakuwa tena chakula chao.

11 [k]" 'Kwa kuwa hili ndilo BWANA Mwenyezi asemalo: Mimi mwenyewe nitawaulizia kondoo wangu na kuwatafuta. 12 [l]Kama vile mchungaji atafutavyo kundi lake lililotawanyika wakati akiwa pamoja nalo, hivyo ndivyo nitakavyowatafuta kondoo wangu. Nitawaokoa kutoka mahali pote walipokuwa wametawanyikia katika siku ya mawingu na giza nene. 13 [m]Nitawatoa katika mataifa na kuwakusanya kutoka nchi mbalimbali, nami nitawaleta katika nchi yao wenyewe. Nitawalisha kwenye milima ya Israeli, katika mabonde na mahali pote panapokalika katika nchi. 14 [n]Nitawachunga kwenye malisho mazuri na miinuko ya mlima wa Israeli patakuwa mahali pao pa malisho. Huko watajipumzisha kwa amani katika nchi ya malisho mazuri, nao watajilisha huko katika malisho tele katika

[a]**33:32** Mk 6:20; Yak 1:22
[b]**33:33** 1Sam 3:20; Yer 28:9; Eze 2:5
[c]**34:2** Mik 3:11; Yud 12; Yer 3:15; Isa 40:11; Za 78:70-72; Yn 21:15-17
[d]**34:3** Amo 6:4; Zek 11:5; Eze 22:27; Isa 56:11
[e]**34:4** Law 25:43; Mik 3:3; 2Tim 2:24; Mdo 9:36; Isa 3:7; Zek 11:15-17
[f]**34:5** Hes 27:17; Isa 56:9; Mdo 20:29
[g]**34:6** Yer 50:6; Law 26:33; Za 95:10; Yer 10:21; 2Nya 18:16; Za 142:4; Hos 7:13; Mt 9:36; 18:12-13
[h]**34:8** 2Nya 18:16; 1Pet 2:25; Yer 50:6; Za 95:10; Yer 10:21; Hos 7:13; Za 42:4; Mt 18:12-13
[i]**34:9** Amu 2:14; Isa 59:6; Yud 12
[j]**34:10** Yer 21:13; Za 72:14; Yer 23:2; Zek 10:3; 1Sam 2:29-30
[k]**34:11** Za 119:176
[l]**34:12** Zek 10:3; Lk 19:10; Eze 30:3; 32:7; Mdo 2:19-21; Isa 40:11
[m]**34:13** Mwa 48:21; Yer 23:3, 8; 50:19; Kum 30:4; Eze 11:17
[n]**34:14** Eze 20:40; 37:22; Za 23:2; 37:3; Isa 65:10; Amo 9:14; Eze 36:29-30

milima ya Israeli. 15 [a]Mimi mwenyewe
nitawachunga kondoo zangu na kuwafanya
wapumzike, asema BWANA Mwenyezi.
16 [b]Nitawaulizia kondoo waliopotea na
kuwaleta waliotangatanga. Nitawafunga
waliojeruhiwa na kuwatia nguvu walio
dhaifu lakini wale waliojikinai na wenye
nguvu nitawaangamiza. Nitalichunga kundi
kwa haki.
17 [c]“ ‘Kwa habari yenu, enyi kundi langu,
hili ndilo BWANA Mwenyezi asemalo:
Nitahukumu kati ya kondoo na kondoo,
kati ya kondoo dume na mbuzi. 18 [d]Je,
haiwatoshi ninyi kujilisha kwenye malisho
mazuri? Je, ni lazima ninyi kuyakanyaga
pia malisho yenu yaliyobaki kwa miguu
yenu? Je, haiwatoshi ninyi kunywa maji
safi? Je, ni lazima kuyachafua maji mengine
kwa miguu yenu? 19 Je, ni lazima kundi
langu wajilishe kwa yale mliyoyakanyaga
na kunywa maji mliyoyachafua kwa miguu
yenu?
20 [e]“ ‘Kwa hiyo, hili ndilo BWANA
Mwenyezi awaambialo: Tazama, mimi
mwenyewe nitahukumu kati ya kondoo
wanono na waliokonda. 21 [f]Kwa sababu
mmewapiga kikumbo na kuwapiga kwa
pembe zenu kondoo wote walio dhaifu
mpaka wakawafukuza, 22 [g]nitaliokoa
kundi langu na hawatatekwa nyara tena.
Nitahukumu kati ya kondoo na kondoo.
23 [h]Nitaweka juu yao mchungaji mmoja,
mtumishi wangu Daudi, naye atawachunga,
atawachunga na kuwa mchungaji wao.
24 [i]Mimi BWANA nitakuwa Mungu wao,
naye mtumishi wangu Daudi atakuwa mkuu
miongoni mwao. Mimi BWANA nimenena.

25 [j]“ ‘Nitafanya nao Agano la amani na
kuwaondoa wanyama wa mwitu kutoka
nchi yao ili kondoo wangu waweze
kupumzika nyikani na msituni kwa
salama. 26 [k]Nitawabariki wao pamoja na
maeneo yanayozunguka kilima changu.
Nitawanyeshea mvua kwa majira yake,
kutakuwepo mvua za baraka. 27 [l]Miti ya
shambani itatoa matunda yake na ardhi
itatoa mazao yake, watu watakaa salama
katika nchi yao. Watajua kuwa Mimi ndimi
BWANA, nitakapovunja vifungo vya nira
zao na kuwaokoa kutoka mikono ya wale
waliowafanya watumwa. 28 [m]Hawatatekwa
tena nyara na mataifa, wala wanyama pori
hawatawala tena. Wataishi kwa salama,
wala hakuna yeyote atakayewatia hofu.
29 [n]Nitawapa nchi yenye sifa kutokana na
mazao yake, hawatapatwa na njaa katika
nchi tena wala hawatadharauliwa na
mataifa. 30 [o]Ndipo watakapojua kuwa Mimi,
BWANA, Mungu wao, niko pamoja nao, na
kwamba wao, nyumba ya Israeli, ni watu
wangu, asema BWANA Mwenyezi. 31 [p]Ninyi
ni kondoo wangu, kondoo wa malisho
yangu, ninyi ni watu wangu, nami ni
Mungu wenu, asema BWANA Mwenyezi.’ ”

### *Unabii Dhidi Ya Edomu*

35 Neno la BWANA likanijia kusema:
2 [q]“Mwanadamu, elekeza uso wako
juu ya mlima Seiri, utabiri dhidi yake
3 [r]na useme: ‘Hili ndilo BWANA Mwenyezi
asemalo: Mimi ni kinyume nawe, ee mlima
Seiri, nami nitanyoosha mkono wangu dhidi
yako na kukufanya ukiwa na usiyekaliwa na

[a]**34:15** Sef 3:13; Mik 5:4; Za 23:1-2; Yer 33:12
[b]**34:16** Isa 61:1-2; Mik 4:6; Sef 3:19; Yer 31:8; Lk 5:32; Mt 2:17; 15:24
[c]**34:17** Mt 25:32-33; Eze 20:37
[d]**34:18** Mwa 30:15; Eze 32:2
[e]**34:20** Eze 34:17
[f]**34:21** Kum 33:17
[g]**34:22** Za 72:12-14; Yer 23:2-3; Eze 20:37-38
[h]**34:23** Ebr 13:20; Isa 40:11; Eze 37:24; Isa 31:4; Mik 5:4
[i]**34:24** Eze 36:28; Yer 33:14; 30:4; Yn 10:16; Kut 29:45; Za 89:49; Isa 53:4; Ufu 7:17
[j]**34:25** Law 26:6; 25:18; Hos 2:18; Yer 23:6; Isa 11:6-9; Hes 25:12; Eze 16:62
[k]**34:26** Mwa 12:2; Za 68:9; Yoe 2:23; Kum 28:12; 11:13-15
[l]**34:27** Yer 2:20; Law 26:13; Yer 30:8; Eze 20:42; Yer 25:14; Za 72:16; Ay 14:9
[m]**34:28** Hos 11:11; Zek 14:11; Amo 9:15; Yer 30:10; 32:37; Eze 28:26; 39:26
[n]**34:29** Isa 4:2; Yoe 2:19; Eze 36:15, 29; Za 137:3
[o]**34:30** Eze 14:11; 37:27; 2Tim 1:12
[p]**34:31** Za 100:3; Yer 23:1; Za 28:9
[q]**35:2** Mwa 14:6; Kum 2:5; Yer 49:7-8; Amo 1:11
[r]**35:3** Yer 6:12; Eze 34:10; 25:12-14; Oba 1:10

watu wala kulimika. [4] [a]Nitaifanya miji yako
kuwa magofu nawe utakuwa ukiwa. Ndipo
utakapojua kuwa Mimi ndimi BWANA.
[5] [b]“ ‘Kwa sababu ulificha moyoni uadui
wa siku nyingi nawe ukawatoa Waisraeli
wauawe kwa upanga wakati wa maafa
yao, wakati adhabu yake ilipofikia kilele
chake, [6] [c]kwa hiyo hakika kama niishivyo,
asema BWANA Mwenyezi, nitakutia
katika umwagaji damu nao utakufuatia.
Kwa kuwa hakuchukia kumwaga damu,
kumwaga damu kutakufuatia. [7] [d]Nitaufanya
Mlima Seiri ukiwa na usiokaliwa na
watu wala kulimika na kuukatilia mbali
na wote wanaokuja na wanaokwenda.
[8] [e]Nitaijaza milima yenu kwa watu wake
waliouawa, wale waliouawa kwa upanga
wataanguka juu ya vilima vyako na katika
mabonde yako na katika makorongo
yako yote. [9] [f]Nitakufanya ukiwa milele,
watu hawataishi katika miji yako. Ndipo
utakapojua kuwa Mimi ndimi BWANA.
[10] [g]“ ‘Kwa sababu umesema, “Mataifa
haya mawili na nchi hizi zitakuwa zetu
nasi tutazimiliki,” ingawa hata mimi
BWANA nilikuwa huko, [11] [h]kwa hiyo hakika
kama niishivyo, asema BWANA Mwenyezi,
nitakutenda kwa kadiri ya hasira na wivu
uliouonyesha katika chuki yako juu yao
nami nitafanya nijulikane miongoni mwao
wakati nitakapokuhukumu. [12] [i]Ndipo
utakapojua kuwa Mimi BWANA nimesikia
mambo yote ya dharau uliyosema dhidi ya
milima ya Israeli. Ulisema, “Wamefanyika
ukiwa na kutiwa mikononi mwetu
tuwararue.” [13] [j]Ulijigamba dhidi yangu
na kusema maneno dhidi yangu bila
kujizuia, nami nikayasikia. [14] [k]Hili ndilo
BWANA Mwenyezi asemalo: Wakati dunia
yote inashangilia nitakufanya ukiwa.
[15] [l]Kwa sababu ulishangilia wakati urithi
wa nyumba ya Israeli ulipofanyika ukiwa,
hivyo ndivyo nitakavyokutendea. Utakuwa
ukiwa, ee mlima Seiri, wewe na Edomu
yote. Kisha ndipo watajua kuwa Mimi ndimi
BWANA.’ ”

### *Unabii Kwa Milima Ya Israeli*

36 [m]“Mwanadamu, itabirie milima ya
Israeli na useme, ‘Ee milima ya
Israeli, sikieni neno la BWANA. [2] [n]Hili
ndilo BWANA Mwenyezi asemalo: Kwa
sababu adui wanasema juu yako, “Aha!
Mahali palipoinuka pa zamani pamekuwa
milki yetu.” ’ [3] [o]Kwa hiyo tabiri na useme,
‘Hili ndilo BWANA Mwenyezi asemalo:
Kwa sababu wamewafanya ukiwa na
kuwagandamiza kila upande ili mpate kuwa
milki ya mataifa mengine na kuwa kitu cha
kusimangwa na kudhihakiwa miongoni
mwa watu, [4] [p]kwa hiyo, ee milima ya Israeli,
sikieni neno la BWANA Mwenyezi: Hili ndilo
BWANA Mwenyezi asemalo kwa milima na
vilima, kwa makorongo na mabonde, kwa
mahame yaliyo ukiwa, miji iliyoachwa
ambayo imetekwa nyara na kudharauliwa
na mataifa mengine yanayowazunguka,
[5] [q]hili ndilo BWANA Mwenyezi asemalo:
Katika wivu wangu uwakao nimenena dhidi
ya mataifa mengine na dhidi ya Edomu
yote, kwa maana kwa furaha na hila katika
mioyo yao waliifanya nchi yangu kuwa
milki yao ili wapate kuteka nyara sehemu
yake ya malisho.’ [6] [r]Kwa hiyo tabiri kuhusu
nchi ya Israeli na uiambie milima na vilima,
makorongo na vijito na mabonde: ‘Hili
ndilo BWANA Mwenyezi asemalo: Ninanena

[a]**35:4** Yer 49:10; 44:2
[b]**35:5** Za 137:7; Eze 21:29; Za 63:10; Oba 1:13
[c]**35:6** Isa 63:2-6; 34:3
[d]**35:7** Yer 46:19; 49:17
[e]**35:8** Eze 31:12
[f]**35:9** Isa 34:5-6; Yer 49:13-17; Oba 1:10
[g]**35:10** Za 83:12; Eze 36:2-5
[h]**35:11** Eze 25:14; Oba 1:15; Mt 7:2; Isa 26:9; Za 9:16
[i]**35:12** Yer 50:7; Za 9:16
[j]**35:13** Dan 11:36; Yer 49:16
[k]**35:14** Yer 51:48
[l]**35:15** Mit 17:5; Eze 36:5; Oba 1:12; Mao 4:4-21; Yer 50:11-13; Isa 34:5-6; Eze 32:29
[m]**36:1** Eze 6:2, 3; 17:22
[n]**36:2** Eze 25:3; Kum 32:13; Eze 35:10; Hab 3:19; Eze 6:2-3
[o]**36:3** Za 44:12-14; Mao 3:62; Oba 1:13; Mao 2:16
[p]**36:4** Eze 6:3; Kum 11:11; Za 79:4; Eze 33:24; Law 26:43; Yer 2:26; Eze 33:28-29
[q]**36:5** Kum 4:24; Isa 66:16; Yoe 3:2-14; Zek 1:15; Yer 25:31; Kum 29:20
[r]**36:6** Za 123:3-4; Eze 34:29

katika wivu wa ghadhabu yangu kwa
sababu mmedharauliwa na mataifa. 7 [a]Kwa
hiyo hili ndilo BWANA Mwenyezi asemalo:
Ninaapa kwa mkono wangu ulioinuliwa
kwamba mataifa wanaowazunguka nao pia
watadharauliwa.

8 [b]“ ‘Lakini ninyi, ee milima ya Israeli,
mtatoa matawi na matunda kwa ajili
ya watu wangu Israeli, kwa sababu hivi
karibuni watakuja nyumbani. 9 Mimi
ninawajibika nanyi na nitawaangalia
kwa upendeleo, mtalimwa na kupandwa
mbegu, 10 [c]nami nitaizidisha idadi ya watu
kwenu, naam, nyumba yote ya Israeli. Miji
itakaliwa na watu na magofu yatajengwa
upya. 11 [d]Nitaongeza idadi ya watu na
wanyama juu yenu, nao watazaana sana
na kuwa wengi mno. Nitawakalisha watu
ndani yenu kama ilivyokuwa wakati
uliopita, nami nitawafanya mfanikiwe
kuliko hapo kwanza. Ndipo mtakapojua
kuwa Mimi ndimi BWANA. 12 [e]Nitawafanya
watu, watu wangu Israeli, kutembea juu
yenu. Watawamiliki ninyi, nanyi mtakuwa
urithi wao, kamwe hamtawaondolea tena
watoto wao.

13 [f]“ ‘Hili ndilo BWANA Mwenyezi
asemalo: Kwa sababu watu wanakuambia,
“Unawala watu na kuliondolea taifa lako
watoto wake,” 14 kwa hiyo hutakula tena
watu wala kulifanya tena taifa lako lisiwe
na watoto, asema BWANA Mwenyezi.
15 [g]Sitakufanya tena usikie dhihaka za
mataifa, wala kudharauliwa na kabila za
watu, wala kulifanya taifa lako lianguke,
asema BWANA Mwenyezi.’ ”

16 Neno la BWANA likanijia tena, kusema:
17 [h]“Mwanadamu, nyumba ya Israeli
walipokuwa wakiishi katika nchi yao
wenyewe, waliinajisi kwa mwenendo wao
na matendo yao. Mwenendo wao mbele
zangu ulikuwa kama mwanamke aliye
katika hedhi. 18 [i]Hivyo nilimwaga ghadhabu
yangu juu yao kwa sababu walikuwa
wamemwaga damu katika nchi na kwa
sababu walikuwa wameitia nchi unajisi kwa
sanamu zao. 19 [j]Nikawatawanya miongoni
mwa mataifa, nao wakaenda huku na huko
katika nchi mbalimbali, nikawahukumu
sawasawa na mwenendo wao na matendo
yao. 20 [k]Tena popote walipokwenda
miongoni mwa mataifa walilitia unajisi Jina
langu takatifu, kwa kuwa watu walisema
kuwahusu, ‘Hawa ndio watu wa BWANA,
lakini imewapasa kuondoka katika nchi
yake.’ 21 [l]Lakini niliwahurumia kwa ajili
ya Jina langu takatifu, ambalo nyumba
ya Israeli imelitia unajisi miongoni mwa
mataifa huko walikokwenda.

22 [m]“Kwa hiyo iambie nyumba ya Israeli,
‘Hili ndilo BWANA Mwenyezi asemalo:
Si kwa ajili yako, ee nyumba ya Israeli,
kwamba ninafanya mambo haya, bali ni
kwa ajili ya Jina langu takatifu, ambalo
mmelitia unajisi miongoni mwa mataifa
mliyoyaendea. 23 [n]Nitauonyesha utakatifu
wa Jina langu kuu, ambalo limetiwa
unajisi miongoni mwa mataifa, jina
ambalo limetiwa unajisi miongoni mwao.
Ndipo mataifa watakapojua kuwa Mimi
ndimi BWANA, asema BWANA Mwenyezi,
nitakapojionyesha mwenyewe kuwa
mtakatifu kwa kuwapitia ninyi mbele ya
macho yao.

24 [o]“ ‘Kwa kuwa nitawaondoa ninyi
toka mataifa, nitawakusanya kutoka nchi
zote na kuwarudisha kwenye nchi yenu

[a]**36:7** Yer 25:9; Hes 14:30
[b]**36:8** Isa 4:2; 27:6; Eze 20:5; 47:12
[c]**36:10** Isa 49:17-23; Yer 30:18; Isa 61:4; Amo 9:14
[d]**36:11** Mik 7:14; Law 26:9; Ay 42:13; Hos 2:20; 1Nya 5:20; Yer 31:28; Zek 10:8
[e]**36:12** Eze 47:14; Oba 1:17
[f]**36:13** Hes 13:32
[g]**36:15** Isa 54:4; Za 89:50-51; Sef 3:19-20; Eze 34:29
[h]**36:17** Za 106; 37:38; Law 15:19; Yer 2:7; Law 12:2; Yer 2:7
[i]**36:18** 2Nya 34:21; Eze 16:36, 38; 23:37
[j]**36:19** Kum 28:64; Law 18:24-28; Eze 7:8; 24:14; 39:24
[k]**36:20** Law 18:21; Rum 2:24; Isa 52:5; Yer 33:24; 42:10; Eze 17:22; 12:16
[l]**36:21** Za 74:18; Isa 48:9
[m]**36:22** Rum 2:24; Kum 9:5-6; Za 106:8; Eze 20:9; Kum 9:5-6; Isa 37:35
[n]**36:23** Isa 5:16; 37:23; Za 46:10; 126:2; Eze 20:14; 20:41; Hes 6:27
[o]**36:24** Isa 43:5-6; Eze 34:13; 37:21

wenyewe. 25 [a]Nitawanyunyizia maji safi,
nanyi mtakuwa safi, nitawatakasa kutoka
uchafu wenu wote na kutoka sanamu zenu
zote. 26 [b]Nitawapa moyo mpya na kuweka
roho mpya ndani yenu, nitaondoa ndani
yenu moyo wenu wa jiwe na kuwapa moyo
wa nyama. 27 [c]Nami nitaweka Roho yangu
ndani yenu na kuwafanya ninyi mfuate
amri zangu na kuwafanya kuwa waangalifu
kuzishika sheria zangu. 28 [d]Mtaishi katika
nchi niliyowapa baba zenu, ninyi mtakuwa
watu wangu nami nitakuwa Mungu wenu.
29 [e]Nitawaokoa ninyi kutoka unajisi wenu
wote. Nitaiita nafaka na kuiongeza iwe
nyingi sana nami sitaleta njaa juu yenu.
30 [f]Nitaongeza matunda ya miti na mazao ya
mashamba, ili kwamba msipate tena aibu
miongoni mwa mataifa kwa ajili ya njaa.
31 [g]Ndipo mtakapozikumbuka njia zenu
za uovu na matendo yenu maovu, nanyi
mtajichukia wenyewe kwa ajili ya dhambi
zote na matendo yenu ya kuchukiza.
32 [h]Ninataka ninyi mjue kwamba sifanyi hili
kwa ajili yenu, asema BWANA Mwenyezi.
Oneni aibu na mkatahayari kwa ajili ya
mwenendo wenu, ee nyumba ya Israeli!
33 [i]" 'Hili ndilo BWANA Mwenyezi
asemalo: Siku ile nitakapowasafisha kutoka
dhambi zenu zote, nitarudisha watu waishi
katika miji yenu na magofu yatajengwa
upya. 34 [j]Nchi iliyokuwa ukiwa italimwa
badala ya kukaa ukiwa machoni mwa wale
wote wanaopita ndani yake. 35 [k]Watasema,
"Hii nchi iliyokuwa imeachwa ukiwa sasa
imekuwa kama bustani ya Edeni, miji ile
iliyokuwa magofu, ukiwa na kuangamizwa,
sasa imejengewa ngome na kukaliwa na
watu." 36 [l]Ndipo mataifa yanayowazunguka
yaliyobakia watakapojua kuwa Mimi
BWANA nimejenga tena kile kilichoharibiwa
na nimepanda tena kile kilichokuwa ukiwa.
Mimi BWANA nimenena, nami nitalifanya.'
37 [m]"Hili ndilo BWANA Mwenyezi asemalo:
Mara nyingine tena nitasikia maombi ya
nyumba ya Israeli na kuwatendea jambo
hili: Nitawafanya watu wake kuwa wengi
kama kondoo, 38 [n]kuwa wengi kama kundi
la kondoo kwa ajili ya dhabihu huko
Yerusalemu wakati wa sikukuu zao za
wakati ulioamriwa. Hivyo ndivyo miji
iliyokuwa magofu itajazwa na makundi
ya watu. Ndipo watakapojua kuwa Mimi
ndimi BWANA."

*Bonde La Mifupa Mikavu*

37 [o]Mkono wa BWANA ulikuwa juu yangu,
naye akanitoa nje kwa Roho wa BWANA
na kuniweka katikati ya bonde lililokuwa
limejaa mifupa tele. 2 Akanipitisha
pande zote kwenye hiyo mifupa, nami
nikaona mifupa mingi sana ndani ya lile
bonde, mifupa iliyokuwa imekauka sana.
3 [p]Akaniuliza, "Mwanadamu, mifupa hii
yaweza kuishi?"
Nikajibu, "Ee BWANA Mwenyezi, wewe
peke yako wajua."
4 [q]Ndipo akaniambia, "Itabirie mifupa hii
na uiambie, 'Enyi mifupa mikavu, sikieni
neno la BWANA! 5 [r]Hili ndilo BWANA
Mwenyezi asemalo kwa hii mifupa:
Nitatia pumzi[s] ndani yenu, nanyi mtaishi.
6 [t]Nitawawekea mishipa, nami nitaifanya

[a]**36:25** Ebr 9:13; 10:22; Law 14:7; Zek 3:4; Za 51:2-7; Mdo 22:16; Yoe 3:21
[b]**36:26** Yer 24:7; Za 51:10; 2Kor 3:3, 18; Yn 3:3-5; Eze 18:31
[c]**36:27** Efe 1:13; Yoe 2:29; Yn 3:5; Rum 8:4-9; Eze 37:14; Isa 44:3; Yer 50:20
[d]**36:28** Yer 30:22; 31:33; Eze 11:17; 14:11; 34:24; 37:14; Zek 8:8
[e]**36:29** Eze 34:29; Mt 1:21; Rum 11:26; Za 105:16
[f]**36:30** Law 26:4-5; Hos 2:21-22; Eze 34:13-14
[g]**36:31** Isa 6:5; Yer 31:19; Eze 6:9; 34:13-14
[h]**36:32** Dan 9:19; Kum 9:5
[i]**36:33** Rum 8:30-32; Isa 49:8; Law 16:30; 26:31
[j]**36:34** Yer 51:3
[k]**36:35** Mwa 2:8; Isa 51:3; Yoe 2:3; Amo 9:14
[l]**36:36** Eze 3:26-27; 24:27; 29:21; 17:22; Lk 1:64; Yer 42:10
[m]**36:37** Zek 10:6; 13:9; 13:9; Yer 29:12-14
[n]**36:38** 1Fal 8:63; 2Nya 35:7-9; Kut 6:2
[o]**37:1** Eze 8:3; 11:24; Yer 7:32; 40:1; Lk 4:1; Yer 8:2; Mdo 8:39
[p]**37:3** 1Sam 2:6; 1Kor 15:35; Rum 4:17; Isa 26:19
[q]**37:4** Yer 22:29; Rum 10:17
[r]**37:5** Mwa 2:7; Ufu 11:11
[s]5 Pumzi pia ina maana ya roho kwa Kiebrania.
[t]**37:6** Kut 6:2; Yoe 2:27; Eze 38:23

nyama ije juu yenu na kuwafunika kwa
ngozi. Nitatia pumzi ndani yenu, nanyi
mtakuwa hai. Ndipo mtakapojua kuwa
Mimi ndimi BWANA.' "
7 Basi nikatabiri kama nilivyoamriwa.
Wakati nilipokuwa ninatabiri, kukawa na
sauti, sauti ya kugongana, nayo mifupa
ikasogeleana, mfupa kwa mfupa mwenziwe.
8 Nikatazama, mishipa na nyama vikatokea
juu ya mifupa na ngozi ikaifunika, lakini
hapakuwepo pumzi ndani yake.
9 [a]Ndipo aliponiambia, "Utabirie upepo,
tabiri, mwanadamu na uuambie, 'Hili
ndilo BWANA Mwenyezi asemalo: Njoo
kutoka pande nne, ee pumzi, nawe upulizie
pumzi ndani ya hawa waliouawa, ili
wapate kuishi.' " 10 [b]Hivyo nikatabiri kama
alivyoniamuru, nayo pumzi ikawaingia,
wakawa hai na wakasimama kwa miguu
yao, jeshi kubwa mno.
11 [c]Ndipo akaniambia: "Mwanadamu,
mifupa hii ni nyumba yote ya Israeli. Nao
wanasema, 'Mifupa yetu imekauka na
tumaini letu limetoweka, tumekatiliwa
mbali.' 12 [d]Hivyo watabirie na uwaambie:
'Hili ndilo BWANA Mwenyezi asemalo: Enyi
watu wangu, nitayafunua makaburi yenu na
kuwatoa ndani yake, nami nitawarudisha
tena katika nchi ya Israeli. 13 [e]Ndipo ninyi
watu wangu, mtakapojua kuwa Mimi
ndimi BWANA, nitakapoyafunua makaburi
yenu na kuwatoa humo. 14 [f]Nitatia Roho
yangu ndani yenu nanyi mtaishi, nami
nitawakalisha katika nchi yenu wenyewe.
Ndipo mtakapojua kwamba Mimi BWANA
nimenena, nami nitalitenda, asema
BWANA!' "

*Taifa Moja Chini Ya Mfalme Mmoja*

15 Neno la BWANA likanijia kusema:
16 [g]"Mwanadamu, chukua fimbo na uandike
juu yake, 'Hii ni kwa ajili ya Yuda na
Waisraeli waliofungamana naye.' Kisha
chukua fimbo nyingine, uandike juu yake,
'Fimbo ya Efraimu, ni kwa ajili ya Yosefu
na nyumba yote ya Israeli wanaofungamana
naye.' 17 [h]Ziunganishe pamoja kuwa fimbo
moja ili kwamba ziwe fimbo moja katika
mkono wako.
18 [i]"Watu wako watakapokuuliza, 'Je,
hutatuambia ni nini maana ya jambo
hili?' 19 [j]Waambie, 'Hili ndilo BWANA
Mwenyezi asemalo: Nitaichukua fimbo ya
Yosefu, iliyoko mikononi mwa Efraimu na
ya makabila ya Israeli yanayofungamana
naye na kuiunganisha na fimbo ya
Yuda, nikizifanya kuwa fimbo moja, nao
watakuwa wamoja katika mkono wangu.'
20 [k]Inua mbele ya macho yao zile fimbo
ulizoziandika 21 [l]kisha waambie, 'Hili ndilo
BWANA Mwenyezi asemalo: Nitawatoa
Waisraeli katika mataifa walikokuwa
wamekwenda. Nitawakusanya popote
walipo na kuwarudisha katika nchi yao
wenyewe. 22 [m]Nitawafanya kuwa taifa
moja katika nchi, katika milima ya Israeli.
Patakuwa na mfalme mmoja juu yao wote
na kamwe hawatagawanyika tena kuwa
mataifa mawili au kugawanyika katika
falme mbili. 23 [n]Hawatajitia tena unajisi
kwa sanamu zao na vinyago vyao visivyo
na maana wala kwa makosa yao yoyote,
kwa maana nitawaokoa kutoka dhambi
zao zote zilizowarudisha nyuma, nami
nitawatakasa. Wao watakuwa watu wangu,
nami nitakuwa Mungu wao.
24 [o]" 'Mtumishi wangu Daudi atakuwa
mfalme juu yao, nao wote watakuwa na

[a]**37:9** Isa 32:15; Zek 12:10; Eze 39:29; Za 104:30; Yer 49:36; Zek 6:5; Dan 7:2
[b]**37:10** Ufu 11:11; Eze 12:7
[c]**37:11** Ay 17:15; Mao 3:54; Isa 49:14
[d]**37:12** Sef 3:20; Yer 29:14; Amo 9:14; 1Sam 2:9; Kum 32:39; Isa 26:19; Hos 13:14
[e]**37:13** Kut 6:2; Eze 17:24; Hos 13:14
[f]**37:14** Isa 11:2; Yoe 2:28-29; Eze 36:27-28; Yer 43:2; Ufu 11:11
[g]**37:16** Hes 17:2; 1Fal 12:20; 2Nya 10:17-19; 15:9
[h]**37:17** Isa 11:13; Hos 1:11; Yer 50:4
[i]**37:18** Eze 24:19; 12:9
[j]**37:19** Zek 10:6
[k]**37:20** Eze 12:3
[l]**37:21** Isa 43:5-6; Mik 4:6; Eze 20:42; 39:27
[m]**37:22** Isa 11:13; Yer 3:18; Yn 10:16; Eze 17:22; 34:13-14; Yer 33:24
[n]**37:23** Isa 2:18; Nah 2:2; Eze 11:18; Hos 14:8; Zek 13:2-3; Yer 7:24; Eze 43:7
[o]**37:24** Isa 55:4; Hos 3:5; Amo 9:15; Za 78:70-71; Yer 30:21; 1Sam 13:14

mchungaji mmoja. Watafuata sheria zangu
na kuzishika amri zangu kwa uangalifu.
25 [a]Wataishi katika nchi niliyompa mtumishi
wangu Yakobo, nchi ambamo baba zenu
waliishi. Wao na watoto wao na watoto
wa watoto wao wataishi humo milele, naye
Daudi mtumishi wangu atakuwa mkuu wao
milele. 26 [b]Nitafanya nao Agano la amani,
litakuwa Agano la milele. Nitawafanya
imara na kuongeza idadi yao, nami
nitaweka mahali patakatifu pangu miongoni
mwao milele. 27 [c]Maskani yangu yatakuwa
pamoja nao, nitakuwa Mungu wao, nao
watakuwa watu wangu. 28 [d]Ndipo mataifa
watakapojua kwamba Mimi Bwana ndiye
ninayeifanya Israeli kuwa takatifu, wakati
mahali patakatifu pangu patakapokuwa
miongoni mwao milele.' "

*Unabii Dhidi Ya Gogu*

38 Neno la Bwana likanijia kusema:
2 [e]"Mwanadamu, kaza uso wako dhidi
ya Gogu, katika nchi ya Magogu, mkuu wa
Roshi, Mesheki na Tubali, tabiri dhidi yake
3 [f]na useme: 'Hili ndilo Bwana Mwenyezi
asemalo: Ee Gogu, mimi ni kinyume nawe,
mtawala mkuu wa Roshi, Mesheki na
Tubali. 4 [g]Nitakugeuza kuelekea ulikotoka
na kukutia ndoana kwenye mataya yako
na kukutoa nje wewe pamoja na jeshi
lako lote, yaani, farasi wako, wapanda
farasi wako waliojiandaa tayari kwa vita,
pamoja na kundi kubwa la wajeuri wakiwa
na ngao na vigao, wote wakipunga panga
zao. 5 [h]Uajemi, Kushi[i] na Putu watakuwa
pamoja nao, wote wakiwa na ngao na kofia
za chuma, 6 [j]pia Gomeri pamoja na vikosi
vyake vyote, na Beth-Togarma kutoka
kaskazini ya mbali pamoja na vikosi vyake
vyote, mataifa mengi wakiwa pamoja nawe.
7 [k]" 'Jiandae, uwe tayari, wewe na makundi
yako yote ya wajeuri yaliyokusanyika
pamoja nawe, nawe waamrishe. 8 [l]Baada
ya siku nyingi utaitwa vitani. Katika
miaka ijayo, utaivamia nchi ile ambayo
imepona kutoka vita, ambayo watu wake
walikusanywa kutoka mataifa mengi kuja
katika milima ya Israeli, ambayo kwa
muda mrefu ilikuwa imeachwa ukiwa.
Wameletwa kutoka mataifa na sasa wote
wanaishi katika hali ya salama. 9 [m]Wewe na
vikosi vyako vyote na mataifa mengi yaliyo
pamoja nawe mtapanda juu, mtawazoa
kama tufani na kuifunika nchi kama wingu.
10 [n]" 'Hili ndilo Bwana Mwenyezi
asemalo: Katika siku ile mawazo yataingia
moyoni mwako nawe utapanga mipango
mibaya. 11 [o]Utasema, "Nitapigana vita na
nchi ambayo vijiji vyake havina maboma.
Nitawashambulia watu wanaoishi kwa
amani na wasiotarajia vita: wote wanaishi
bila maboma na bila malango na makomeo.
12 Nitateka mateka na kuchukua nyara
mali za wale waliorudi kuishi katika
mahame na wale watu waliokusanywa
kutoka kwa mataifa, ambao sasa wana
mifugo na mali nyingi, wanaoishi katikati
ya nchi." 13 [p]Sheba na Dedani pamoja na
wafanyabiashara wa Tarshishi na vijiji
vyake vyote watakuambia, "Je, umekuja
kuteka mateka? Je, umekusanya makundi
yako ya wajeuri ili kuchukua nyara mali,
kutwaa fedha na dhahabu, kutunyang'anya
mifugo na mali na kuteka nyara nyingi
zaidi?" '

[a]**37:25** Ezr 9:12; Amo 9:15; Za 89:3-4; Eze 28:25; Isa 11:1; Eze 34:23-24
[b]**37:26** Hes 25:12; Isa 55:3; Yer 30:19; Eze 16:62; Mwa 9:16; Kum 29:14
[c]**37:27** Law 26:11; Yn 1:14; Eze 34:30; 2Kor 6:16; Eze 36:28
[d]**37:28** Kut 31:13; Eze 20:12; Hos 1:10-11; Eze 43:9; Sef 3:15
[e]**38:2** Mwa 10:2; Eze 27:13; Ufu 20:8; Eze 39:11
[f]**38:3** Eze 39:1
[g]**38:4** 2Fal 19:28; Isa 43:17; Dan 11:40; Eze 23:12; 29:4; 39:2
[h]**38:5** Eze 27:10-14; Mwa 10:6
[i]5 Kushi ni Ethiopia.
[j]**38:6** Mwa 10:2-3; Eze 32:30
[k]**38:7** Isa 8:9; 8:10; Yer 46:3, 4, 14; 51:12
[l]**38:8** Isa 11:11; 24:22; Kum 4:30; Yer 23:6; Yoe 3:1; Eze 28:26
[m]**38:9** Isa 25:4; 28:2; Yer 4:13; Yoe 2:2; Ufu 20:8
[n]**38:10** Yer 17:10; Za 36:4; Mik 2:1
[o]**38:11** Yer 49:31; Zek 2:4; Amu 18:7-27; Mwa 34:25
[p]**38:13** Mwa 10:7; Eze 27:22; Isa 33:23; Yer 15:13; Mwa 25:3; Isa 10:6

14 [a]“Kwa hiyo, mwanadamu, tabiri
na umwambie Gogu: ‘Hili ndilo BWANA
Mwenyezi asemalo: Katika siku ile, watu
wangu Israeli watakapokuwa wanaishi
salama, Je, wewe mwenyewe hutalijua hilo?
15 [b]Utakuja kutoka kwako huko kaskazini ya
mbali, ukiwa pamoja na mataifa mengi,
wote wakiwa wamepanda farasi, kundi
kubwa, jeshi kuu. 16 [c]Utakuja dhidi ya watu
wangu Israeli kama wingu lifunikavyo nchi.
Siku zijazo, ee Gogu, nitakuleta wewe dhidi
ya nchi yangu, ili kwamba mataifa wapate
kunijua Mimi nitakapojionyesha mtakatifu
kwa kukupitia wewe mbele ya macho yao.
17 “ ‘Hili ndilo BWANA Mwenyezi
asemalo: Je, wewe si yule niliyenena juu
yako katika siku za zamani kwa kupitia
kwa watumishi wangu manabii wa
Israeli? Wakati ule walitabiri kwa miaka
mingi kwamba ningekuleta upigane nao.
18 Hili ndilo litakalotokea katika siku ile:
Gogu atakaposhambulia nchi ya Israeli,
hasira yangu kali itaamka, asema BWANA
Mwenyezi. 19 [d]Katika wivu wangu na
ghadhabu yangu kali ninasema kuwa
wakati ule patakuwepo tetemeko kuu
katika nchi ya Israeli. 20 [e]Samaki wa
baharini, ndege wa angani, wanyama
wa kondeni, kila kiumbe kitambaacho
ardhini, na watu wote walio juu ya uso
wa nchi watatetemeka mbele zangu. Milima
itapinduka, majabali yatapasuka na kila
ukuta utaanguka chini. 21 [f]Nitaita upanga
vita dhidi ya Gogu juu ya milima yangu
yote, asema BWANA Mwenyezi. Upanga
wa kila mtu utakuwa dhidi ya ndugu yake.
22 [g]Nitatekeleza hukumu juu yake kwa tauni
na kwa umwagaji wa damu. Nitaifanya
mvua ya mafuriko kunyesha, mvua ya
mawe na moto wa kiberiti juu yake na juu
ya vikosi vyake na juu ya mataifa mengi
walio pamoja naye. 23 [h]Nami hivyo ndivyo
nitakavyoonyesha ukuu wangu na utakatifu
wangu, nami nitajijulisha mbele ya macho
ya mataifa mengi. Ndipo watakapojua kuwa
Mimi ndimi BWANA.’

*Majeshi Ya Gogu Yataangamizwa*

39 [i]“Mwanadamu, tabiri dhidi ya Gogu
useme: ‘Hili ndilo BWANA Mwenyezi
asemalo: Ee Gogu mimi ni kinyume nawe,
mtawala mkuu wa Roshi, Mesheki na
Tubali. 2 [j]Nitakugeuza kuelekea ulikotoka
na kukuburuta. Nitakuleta kutoka kaskazini
ya mbali na kukupeleka wewe dhidi ya
milima ya Israeli. 3 [k]Kisha nitaupiga upinde
wako kutoka mkono wako wa kushoto na
kuifanya mishale ianguke kutoka mkono
wako wa kuume. 4 [l]Utaanguka kwenye
milima ya Israeli, wewe pamoja na vikosi
vyako vyote na yale mataifa yaliyo pamoja
nawe. Nitakutoa uwe chakula cha ndege wa
aina zote walao nyama na cha wanyama wa
mwituni. 5 [m]Utaanguka katika uwanja, kwa
kuwa nimenena, asema BWANA Mwenyezi.
6 [n]Nitatuma moto juu ya Magogu na kwa
wale wanaoishi kwa salama huko pwani,
nao watajua kwamba Mimi ndimi BWANA.
7 [o]“ ‘Nitalifanya Jina langu takatifu
lijulikane miongoni mwa watu wangu
Israeli. Sitaliacha tena Jina langu takatifu
litiwe unajisi, nayo mataifa watajua kuwa
Mimi BWANA ndimi Aliye Mtakatifu wa
Israeli. 8 [p]Hili jambo linakuja! Hakika
litatokea, asema BWANA Mwenyezi. Hii
ndiyo siku ile niliyosema habari zake.
9 [q]“ ‘Ndipo wale wanaoishi katika miji

[a]**38:14** Law 25:18; Yer 16:15; Zek 2:5
[b]**38:15** Eze 39:2; Ufu 20:8; Eze 32:30
[c]**38:16** Eze 38:9; 38:8; Kut 14:4; Eze 36:23; 39:21
[d]**38:19** Za 18:7; Hag 2:6, 21; Isa 29:23; Yoe 3:11; Law 10:3
[e]**38:20** Za 76:8; Yer 4:24; Kut 15:14; Isa 42:15; Ay 14:18; Hos 4:3
[f]**38:21** Isa 66:16; Kut 9:18; Ufu 16:21; Yer 25:31; Amu 7:22; 1Sam 14:20; Hag 2:22
[g]**38:22** Yer 25:31; Eze 36:5; 14:19; Kut 9:18; Za 18:12; Ufu 16:21
[h]**38:23** Eze 20:42; 36:23; 37:6
[i]**39:1** Eze 27:13; 38:2; Ufu 20:6
[j]**39:2** Eze 32:30; 38:4, 15
[k]**39:3** Amo 2:15; Za 76:3
[l]**39:4** Yer 25:33; Eze 29:5; Mwa 40:19; Isa 34:2-8
[m]**39:5** Eze 32:4
[n]**39:6** Ufu 20:9; Yer 25:22; Eze 30:8; Kut 6:7
[o]**39:7** Kut 20:7; Eze 13:19; Isa 12:6; 54:5; Eze 20:9; 36:23; Isa 49:26
[p]**39:8** Eze 7:3-8; 38:17
[q]**39:9** Za 46:9; 76:3

ya Israeli watakapotoka na kutumia hizo
silaha kuwashia moto na kuziteketeza,
yaani, kigao na ngao, pinde na mishale,
rungu za vita na mikuki. Kwa miaka saba
watavitumia kama kuni. 10 [a]Hawatahitaji
kukusanya kuni kutoka mashambani wala
kukata kuni kutoka kwenye misitu, kwa
sababu watatumia silaha kuwa kuni. Nao
watawateka mateka wale waliowateka na
kuchukua nyara mali za wale waliochukua
mali zao nyara, asema Bwana Mwenyezi.

11 [b]“ ‘Siku ile nitampa Gogu mahali pa
kuzikia katika Israeli, katika bonde la wale
wasafirio upande wa mashariki kuelekea
baharini. Jambo hili litazuia njia ya wasafiri
kwa sababu Gogu na makundi yake yote ya
wajeuri watazikwa huko. Kwa hiyo litaitwa
Bonde la Hamon-Gogu.[c]

12 [d]“ ‘Kwa miezi saba nyumba ya Israeli
itakuwa ikiwazika ili kuisafisha nchi.
13 [e]Watu wote wa nchi watawazika, nayo
siku nitakayotukuzwa itakuwa siku ya
kumbukumbu kwa ajili yao, asema Bwana
Mwenyezi.

14 [f]“ ‘Watu wataajiriwa mara kwa mara
kuisafisha nchi. Baadhi yao watapita
nchini kote na zaidi yao hao wengine,
watawazika wale waliosalia juu ya uso wa
nchi. Mwisho wa hiyo miezi saba wataanza
upekuzi wao. 15 Wakati wanapopita nchini
kote na mmoja wao akaona mfupa wa
mwanadamu, ataweka alama kando yake
mpaka wachimba kaburi wawe wameuzika
katika Bonde la Hamon-Gogu. 16 [g](Pia mji
uitwao Hamona[h] utakuwa humo.) Hivyo
ndivyo watakavyoisafisha nchi.’

17 [i]“Mwanadamu, hili ndilo Bwana
Mwenyezi asemalo: Ita kila aina ya ndege
na wanyama wote wa mwituni, waambie:
‘Kusanyikeni mje pamoja kutoka pande
zote kwa ajili ya dhabihu ninayowaandalia,
dhabihu kuu katika milima ya Israeli. Huko
mtakula nyama na kunywa damu. 18 [j]Mtakula
nyama za watu mashujaa na kunywa damu
za wakuu wa dunia kana kwamba ni za
kondoo dume na kondoo wake, mbuzi na
mafahali, wote walionona kutoka Bashani.
19 [k]Katika dhabihu ninayoandaa kwa ajili
yenu, mtakula mafuta mpaka mkinai na
kunywa damu mpaka mlewe. 20 [l]Kwenye
meza yangu watajishibisha kwa farasi na
wapanda farasi, watu mashujaa na askari
wa kila aina,’ asema Bwana Mwenyezi.

21 [m]“Nitauonyesha utukufu wangu
miongoni mwa mataifa, nayo mataifa yote
wataiona adhabu nitakayotoa na mkono
wangu nitakaouweka juu yao. 22 Kuanzia
siku ile na kuendelea nyumba ya Israeli
itajua kuwa Mimi ndimi Bwana, Mungu
wao. 23 [n]Na mataifa watajua kuwa nyumba
ya Israeli walikwenda utumwani kwa ajili
ya dhambi yao, kwa sababu hawakuwa
waaminifu kwangu. Hivyo niliwaficha
uso wangu na kuwatia mikononi mwa adui
zao, nao wote wakaanguka kwa upanga.
24 [o]Niliwatendea sawasawa na uchafu wao
na makosa yao, nami nikawaficha uso
wangu.

25 [p]“Kwa hiyo hili ndilo Bwana Mwenyezi
asemalo: Sasa nitamrudisha Yakobo kutoka
utumwani, nami nitawahurumia watu wote
wa Israeli, nami nitakuwa na wivu kwa
ajili ya Jina langu takatifu. 26 [q]Wataisahau
aibu yao na jinsi walivyoonyesha kutokuwa
waaminifu kwangu mimi wakati waliishi
salama katika nchi yao, bila kuwa na mtu
yeyote wa kuwatia hofu. 27 [r]Nitakapokuwa

[a]**39:10** Isa 33:1; Hab 2:8; Isa 14:2; Kut 3:22
[b]**39:11** Eze 38:2; Isa 34:3
[c]11 Hamon-Gogu maana yake Makundi ya wajeuri wa Gogu.
[d]**39:12** Kum 21:23
[e]**39:13** Eze 28:22; Za 126:2
[f]**39:14** Eze 39:12
[g]**39:16** Eze 39:12
[h]16 Hamona maana yake Kundi (la wajeuri).
[i]**39:17** Isa 18:6; Ay 15:23; Ufu 19:17; Eze 32:4
[j]**39:18** Za 22:12; Yer 51:40
[k]**39:19** Law 3:9
[l]**39:20** Yer 12:9; Ufu 19:17-18; Eze 38:4; Isa 56:9
[m]**39:21** Kut 9:16; Isa 37:20; Eze 38:16
[n]**39:23** Isa 1:15; Kum 31:17; Yer 22:8-9; Isa 59:2; Yer 44:23
[o]**39:24** 2Fal 17:23; Dan 9:7; Eze 36:19; 16:53; Yer 4:18
[p]**39:25** Eze 34:13; Yer 30:18; Isa 27:12-13; Eze 16:53; Yer 33:7
[q]**39:26** 1Fal 4:25; Yer 32:37; Isa 17:2; Mik 4:4; Dan 9:16; Eze 38:8
[r]**39:27** Eze 37:21; 38:16; 36:23

nimewarudisha kutoka mataifa na
kuwakusanya kutoka nchi za adui zao,
mimi nitajionyesha kuwa mtakatifu kwa
kupitia kwao machoni mwa mataifa mengi.
28 [a]Ndipo watakapojua kwamba Mimi ndimi
BWANA, Mungu wao, ingawa niliwapeleka
uhamishoni miongoni mwa mataifa,
nitawakusanya tena katika nchi yao
wenyewe, bila kumwacha yeyote nyuma.
29 [b]Sitawaficha tena uso wangu, kwa maana
nitamimina Roho wangu juu ya nyumba ya
Israeli, asema BWANA Mwenyezi."

### *Eneo La Hekalu Jipya*

40 [c]Katika mwaka wa ishirini na tano
wa uhamisho wetu, mwanzoni mwa
huo mwaka, siku ya kumi ya mwezi, katika
mwaka wa kumi na nne baada ya kuanguka
kwa mji, siku hiyo hiyo mkono wa BWANA
ulikuwa juu yangu, naye akanipeleka
huko. 2 [d]Nikiwa katika maono ya Mungu
alinichukua mpaka nchi ya Israeli, naye
akaniweka kwenye mlima mrefu sana,
ambako upande wa kusini kulikuwepo
baadhi ya majengo ambayo yalionekana
kama mji. 3 [e]Akanipeleka huko, nami
nikamwona mtu ambaye kuonekana kwake
kulikuwa kama kuonekana kwa shaba.
Alikuwa amesimama kwenye lango akiwa
na kamba ya kitani na ufito wa kupimia
mkononi mwake. 4 [f]Mtu huyo akaniambia,
"Mwanadamu, angalia kwa macho yako na
usikie kwa masikio yako nawe uzingatie
kitu nitakachokuonyesha, kwa kuwa ndiyo
sababu umeletwa hapa. Iambie nyumba ya
Israeli kila kitu utakachoona."

### *Lango La Mashariki Kuelekea Ukumbi Wa Nje*

5 [g]Nikaona ukuta uliozunguka eneo lote
la Hekalu. Ule ufito wa kupimia uliokuwa
mkononi mwa yule mtu ulikuwa na urefu
wa dhiraa ndefu sita,[h] yaani, dhiraa ndefu
ni sawa na dhiraa na nyanda nne, akapima
ule ukuta. Ukuta huo ulikuwa na unene
wa dhiraa ndefu sita na kimo cha dhiraa
ndefu sita.
6 [i]Kisha akaenda kwenye lango
linaloelekea mashariki. Akapanda ngazi
zake akapima kizingiti cha lango, nacho
kilikuwa na kina cha huo ufito. 7 Vyumba
vya kupumzikia vya walinzi vilikuwa na
urefu wa huo ufito mmoja na upana wa huo
ufito, kuta zilizogawa vyumba hivyo vya
mapumziko zilikuwa na unene wa dhiraa
tano.[j] Nacho kizingiti cha lango lililokuwa
karibu na ukumbi unaoelekea hekaluni
ulikuwa na kina cha huo ufito.
8 Kisha akapima baraza ya njia ya lango,
9 ambayo ilikuwa na kina cha dhiraa nane[k]
na miimo yake ilikuwa na unene wa dhiraa
mbili.[l] Baraza ya lango ilielekea Hekalu.
10 Ndani ya lango la mashariki kulikuwepo
vyumba vitatu vya kupumzikia kila upande,
vyote vitatu vilikuwa na vipimo vilivyo
sawa, nazo nyuso za kuta zilizotenganisha
kila upande zilikuwa na vipimo vilivyo
sawa. 11 Kisha akapima upana wa ingilio
la lango, ilikuwa dhiraa kumi na urefu wake
ulikuwa dhiraa kumi na tatu. 12 Mbele ya
kila chumba cha kupumzikia kulikuwepo
ukuta uliokuwa na kimo cha dhiraa moja[m]
kwenda juu, navyo hivyo vyumba vilikuwa
dhiraa sita mraba. 13 Kisha akapima njia ya
lango kuanzia juu ya ukuta wa nyuma wa
chumba kimoja cha kupumzikia hadi juu
ya ukuta wa nyuma wa chumba upande wa
pili; kukawa na nafasi ya dhiraa ishirini na
tano kuanzia lango la ukuta mmoja hadi
lango la ukuta uliokuwa upande mwingine.
14 [n]Akapima pia ukumbi, urefu wa dhiraa
ishirini[o] na lango linalofuatia hiyo nguzo

---

[a]**39:28** Za 147:2; Eze 36:23, 36
[b]**39:29** Isa 11:2; Mdo 2:27; Hos 2:20; Yoe 2:28; Kum 31:17; Eze 37:9; 16:42
[c]**40:1** 2Fal 25:7; Yer 52:4-11; Eze 29:17; Yer 39:1-10
[d]**40:2** Kut 24:10; Dan 7:7; Yer 31:12; Ufu 21:10
[e]**40:3** Dan 10:6; Ufu 1:15; Zek 2:1-2; Ufu 11:1; Eze 47:3
[f]**40:4** Yer 26:1; Eze 44:5; Kum 6:6
[g]**40:5** Isa 26:1; Eze 42:20
[h]5 Dhiraa ndefu 6 ni sawa na mita 3.18.
[i]**40:6** Eze 8:16
[j]7 Dhiraa 5 ni sawa na mita 2.25.
[k]9 Dhiraa 8 ni sawa na mita 3.6.
[l]9 Dhiraa 2 ni sawa na sentimita 90.
[m]12 Dhiraa 1 ni sawa na sentimita 45.
[n]**40:14** Kut 27:9; Isa 62:9
[o]14 Dhiraa 20 ni sawa na mita 9.

kila upande wa huo ukumbi. 15 Umbali
kuanzia ingilio la njia ya lango hadi mwisho
kabisa wa baraza yake ulikuwa dhiraa
hamsini.[a] 16 [b]Kulikuwa na vidirisha kwenye
hivyo vyumba vya walinzi na nguzo za
hivyo vyumba zilikuwa kwenye mzunguko
wa hilo lango, vivyo hivyo kulikuwa na
madirisha yaliyozunguka kuelekeana na ua
na juu ya kila nguzo kulikuwa na mapambo
ya miti ya mitende.

*Ukumbi Wa Nje*

17 Kisha akanileta katika ukumbi wa nje.
Huko nikaona vyumba vingine pamoja
na njia iliyokuwa imejengwa kuzunguka
ukumbi wote, kulikuwa na vyumba
thelathini vimepangana kando ya hiyo njia.
18 Njia hii iliyojengwa iliambaa na lango,
ikiwa na urefu sawa na lango, hii ilikuwa
ni njia ya chini. 19 [c]Kisha akapima umbali
kutoka ndani ya lango la chini mpaka nje
ya ukumbi wa ndani, nao ulikuwa dhiraa
mia moja[d] upande wa mashariki na dhiraa
mia moja upande wa kaskazini.

*Lango La Kaskazini*

20 Kisha akapima urefu na upana wa lango
linaloelekea kaskazini, kukabili ukumbi wa
nje. 21 [e]Vyumba vyake vilikuwa vitatu kila
upande, kuta zilizogawanya vyumba na
baraza ilikuwa na vipimo sawa na zile kuta
za lango la kwanza. Zilikuwa na urefu wa
dhiraa hamsini na upana wa dhiraa ishirini
na tano.[f] 22 [g]Madirisha yake, baraza yake na
nakshi yake ya miti ya mitende vilikuwa
na vipimo sawasawa na vile vya lango
linaloelekea mashariki. Kulikuwa na ngazi
saba za kupandia huko, pamoja na baraza
yake mkabala nazo. 23 [h]Kulikuwa na lango
kwenye ukumbi wa ndani lililoelekea lile
lango la kaskazini, kama vile ilivyokuwa
ule upande wa mashariki. Akapima kutoka
lango moja hadi lile lililo mkabala nalo,
lilikuwa dhiraa mia moja.

*Lango La Kusini*

24 [i]Ndipo akaniongoza mpaka upande wa
kusini, nami nikaona lango linaloelekea
kusini. Akaipima miimo yake na baraza
yake, navyo vilikuwa na vipimo sawa kama
hivyo vingine. 25 [j]Lango na baraza yake
vilikuwa na madirisha membamba pande
zote, kama madirisha ya huko kwingine.
Ilikuwa na urefu wa dhiraa hamsini
na upana wake dhiraa ishirini na tano.
26 [k]Kulikuwa na ngazi saba za kupandia
huko, pamoja na baraza yake mkabala
nazo. Ilikuwa na nakshi za miti ya mitende
kwenye kuta zilizogawanya vyumba kila
upande. 27 [l]Ukumbi wa ndani pia ulikuwa
na lango lililoelekea kusini. Naye akapima
kutoka lango hili mpaka kwenye lango la
nje upande wa kusini; ilikuwa dhiraa mia
moja.

*Malango Ya Kuelekea Ukumbi Wa Ndani*

28 [m]Kisha akanileta mpaka ukumbi wa
ndani kwa kupitia lango la kusini, naye
akapima lango la kusini, ambalo lilikuwa na
vipimo sawa na yale mengine. 29 [n]Vyumba
vyake, kuta zilizogawanya vyumba na
ukumbi wake zilikuwa na vipimo sawasawa
na zile nyingine. Hilo lango na baraza yake
vilikuwa na madirisha pande zote. Navyo
vilikuwa na urefu wa dhiraa hamsini na
upana wa dhiraa ishirini na tano. 30 [o](Baraza
za malango zilizozunguka ukumbi wa ndani
zilikuwa na upana wa dhiraa ishirini na
tano na kina cha dhiraa tano.) 31 [p]Baraza
yake ilielekeana na ukumbi wa nje, miimo
yake ilinakshiwa miti ya mitende, kulikuwa
na ngazi nane za kupandia huko.

---

[a]15 Dhiraa 50 ni sawa na mita 22.5.
[b]**40:16** 2Nya 3:5; Eze 41:6; 42:1; 1Fal 6:4; Eze 41:26
[c]**40:19** Eze 40:23, 27; 46:1
[d]19 Dhiraa 100 ni sawa na mita 45.
[e]**40:21** Eze 40:7
[f]21 Dhiraa 25 ni sawa na mita 11.25.
[g]**40:22** Eze 40:16, 26, 49
[h]**40:23** Eze 40:19
[i]**40:24** Eze 40:32, 35
[j]**40:25** Eze 40:33
[k]**40:26** Eze 40:22
[l]**40:27** Eze 40:19, 32
[m]**40:28** Eze 40:35
[n]**40:29** 1Fal 6:5-10; 1Nya 28:11-12; Neh 10:38-39
[o]**40:30** Eze 40:21
[p]**40:31** Eze 40:22, 34, 37

32 Kisha akanileta mpaka kwenye ukumbi
wa ndani ulioko upande wa mashariki,
naye akalipima lango hilo, lilikuwa na
vipimo vilivyo sawasawa na yale mengine.
33 [a]Vyumba vyake, kuta zake na baraza yake
vilikuwa na vipimo vilivyo sawa na vile
vingine. Lile lango pamoja na baraza yake
vilikuwa na madirisha pande zote. Urefu
wake ulikuwa dhiraa hamsini na upana
wake dhiraa ishirini na tano. 34 [b]Baraza
yake ilielekea ukumbi wa nje, miimo yake
ilinakshiwa miti ya mitende pande zote.
Kulikuwa na ngazi nane za kupandia huko.
35 [c]Kisha akanileta mpaka kwenye lango
la kaskazini na kulipima. Lilikuwa na
vipimo sawa na yale mengine, 36 [d]kama
vile ilivyokuwa kwa vyumba, kuta zake na
baraza yake, tena kulikuwa na madirisha
pande zote. Ilikuwa na urefu wa dhiraa
hamsini na upana wake dhiraa ishirini na
tano. 37 [e]Baraza yake ilielekeana na ukumbi
wa nje, miimo yake ilinakshiwa miti ya
mitende pande zote, kulikuwa na ngazi
nane za kupandia huko.

*Vyumba Vya Kutayarishia Dhabihu*

38 [f]Kulikuwa na chumba na mlango karibu
na baraza katika kila njia ya ndani ya lango
ambamo sadaka za kuteketezwa zilioshwa.
39 [g]Kwenye baraza ya lile lango kulikuwepo
meza mbili kila upande, ambako sadaka za
kuteketezwa, sadaka za dhambi na sadaka
za hatia zilichinjiwa. 40 Karibu na ukuta wa
nje wa baraza ya lile lango karibu na ngazi
kwenye ingilio kuelekea kaskazini kulikuwa
na meza mbili, nako upande mwingine wa
ngazi kulikuwepo na meza mbili. 41 Kwa
hiyo kulikuwa na meza nne upande mmoja
wa lango na nyingine nne upande mwingine,
zote zilikuwa meza nane, ambapo dhabihu
zilichinjiwa. 42 [h]Pia kulikuwa na meza nne
za mawe yaliyochongwa kwa ajili ya sadaka
za kuteketezwa, kila meza ilikuwa na urefu
wa dhiraa moja na nusu,[i] upana wake
dhiraa moja na nusu na kimo cha dhiraa
moja. Juu ya meza hizo viliwekwa vyombo
vya kuchinjia sadaka za kuteketezwa na
dhabihu nyingine mbalimbali. 43 Kulikuwa
na kulabu, urefu wake nyanda nne,[j] zilikuwa
zimeshikizwa ukutani pande zote. Meza
zilikuwa kwa ajili ya nyama za sadaka.

*Vyumba Kwa Ajili Ya Makuhani*

44 [k]Nje ya lango la ndani, kwenye ukumbi
wa ndani, kulikuwa na vyumba viwili,
kimoja upande wa lango la kaskazini
nacho kilielekea kusini, kingine upande wa
lango la kusini nacho kilielekea kaskazini.
45 [l]Akaniambia, "Chumba kinachoelekea
upande wa kusini ni kwa ajili ya makuhani
ambao wana usimamizi wa hekaluni,
46 [m]nacho chumba kinachoelekea upande
wa kaskazini ni kwa ajili ya makuhani
wenye usimamizi wa madhabahuni. Hawa
ni wana wa Sadoki, ambao ndio Walawi
pekee wanaoweza kumkaribia BWANA ili
kuhudumu mbele zake."
47 [n]Ndipo alipopima ukumbi: nao ulikuwa
mraba wa dhiraa mia moja urefu na upana.
Madhabahu yalikuwa mbele ya Hekalu.

*Hekalu*

48 [o]Akanileta mpaka kwenye baraza ya
Hekalu naye akaipima miimo ya hiyo
baraza, nayo ilikuwa na upana wa dhiraa
tatu[p] kila upande. Upana wa ingilio ulikuwa
dhiraa kumi na nne[q] na kuta zake zilikuwa
na upana wa dhiraa tatu kila upande.
49 [r]Baraza ilikuwa na dhiraa ishirini kwenda

[a]**40:33** Eze 40:7
[b]**40:34** Eze 40:22
[c]**40:35** Eze 44:4; 47:2
[d]**40:36** Eze 40:7
[e]**40:37** Eze 40:22, 34
[f]**40:38** 2Nya 4:6; Eze 42:13; Ebr 9:14
[g]**40:39** Eze 46:2; Law 4:28; Hes 6:12; Ebr 10:12-14; 2Kor 5:21
[h]**40:42** Kut 20:25
[i]42 Dhiraa 1.5 ni sawa na sentimita 67.5.
[j]43 Nyanda 4 ni sawa na sentimita 8.
[k]**40:44** 1Nya 6:31; Kol 3:16; Efe 5:19
[l]**40:45** 1Nya 9:23; Law 8:35
[m]**40:46** Hes 18:5; 16:5; 2Sam 8:17; Eze 48:11; 42:13; Kol 4:12; Eze 43:19; Ezr 7:2; Eze 44:15
[n]**40:47** Eze 41:13-14
[o]**40:48** 1Fal 6:2
[p]48 Dhiraa 3 ni sawa na mita 1.35.
[q]48 Dhiraa 14 ni sawa na mita 6.3.
[r]**40:49** 1Fal 6:3; 7:15

juu na dhiraa kumi na mbili[a] kuanzia mbele
hadi nyuma. Kulikuwa na ngazi kumi za
kupandia huko, pia kulikuwa na nguzo kwa
kila upande wa miimo.

41 [b]Kisha yule mtu akanileta katika
sehemu ya nje ya patakatifu, naye
akaipima miimo; upana wake ulikuwa dhiraa
sita[c] kila upande. 2 [d]Ingilio lilikuwa la upana
wa dhiraa kumi na kuta zilizojitokeza kila
upande zilikuwa na upana wa dhiraa tano.
Pia akapima sehemu ya nje ya patakatifu,
nayo ilikuwa na urefu wa dhiraa arobaini[e]
na upana wa dhiraa ishirini.

3 Kisha akaingia sehemu takatifu ndani
ya Hekalu na kupima miimo ya ingilio,
kila mmoja ulikuwa na upana wa dhiraa
mbili. Ingilio lilikuwa na upana wa dhiraa
sita, na kuta zilizotokeza kila upande
zilikuwa na upana wa dhiraa saba.[f] 4 [g]Naye
akapima urefu wa sehemu takatifu ndani,
nao ulikuwa dhiraa ishirini, na upana
wake ulikuwa dhiraa ishirini hadi mwisho
wa sehemu ya nje ya sehemu takatifu.
Akaniambia, “Hapa ndipo Patakatifu pa
Patakatifu.”

5 Kisha akapima ukuta wa Hekalu,
nao ulikuwa na unene wa dhiraa sita,
na kila chumba cha pembeni kuzunguka
Hekalu kilikuwa na upana wa dhiraa nne.
6 [h]Vyumba vya pembeni vilikuwa na ghorofa
tatu, kimoja juu ya kingine, kila ghorofa
ilikuwa na vyumba thelathini. Kulikuwa
na boriti katika ukuta wote wa Hekalu ili
kuimarisha vyumba vya pembeni, kwa hiyo
boriti hizo hazikushikamanishwa kwenye
ukuta wa Hekalu. 7 [i]Vyumba vya pembeni
vilivyozunguka Hekalu vilizidi kupanuka
kulingana na sakafu zilivyokwenda juu.
Ujenzi uliozunguka Hekalu ulijengwa
kukwea juu, kwa hiyo vyumba vilipanuka
kwa kadiri ya kila kimoja kilivyokwenda
juu. Ngazi za kupandia zilianzia sakafu ya
chini hadi sakafu ya juu kabisa kwa kupitia
sakafu ya kati.

8 [j]Nikaona pia kuwa Hekalu lilikuwa
na kitako kilichoinuliwa pande zote, huu
ulikuwa ndio msingi wa vile vyumba vya
pembeni ambao ulikuwa na urefu wa ule
ufito mmoja wa kupimia, yaani, dhiraa
ndefu sita. 9 Ukuta wa nje wa vyumba
vya pembeni ulikuwa na unene wa dhiraa
tano. Eneo la wazi katikati ya vyumba vya
pembeni vya Hekalu 10 na vyumba vya
makuhani lilikuwa na upana wa dhiraa
ishirini kuzunguka Hekalu pande zote.
11 Kulikuwa na maingilio kwenye vyumba
vya pembeni kutokea eneo lililo wazi, moja
upande wa kaskazini na lingine upande wa
kusini, nao msingi uliounganisha lile eneo
la wazi ulikuwa na upana wa dhiraa tano
ukilizunguka lote.

12 Jengo lililoelekeana na ua wa Hekalu
upande wa magharibi lilikuwa na upana wa
dhiraa sabini. Ukuta wa jengo hilo ulikuwa
na unene wa dhiraa tano, kulizunguka lote,
urefu ulikuwa wa dhiraa tisini.[k]

13 Kisha akapima Hekalu, lilikuwa na
urefu wa dhiraa mia moja na ua wa Hekalu
na jengo pamoja na kuta zake vilikuwa na
urefu wa dhiraa mia moja pia. 14 [l]Upana
wa ua wa Hekalu upande wa mashariki,
pamoja na upande wa mbele wa Hekalu
ulikuwa dhiraa mia moja.

15 [m]Kisha akapima urefu wa jengo
linaloelekeana na ua upande wa nyuma
wa Hekalu, pamoja na vyumba vyake kila
upande, ilikuwa dhiraa mia moja.

Sehemu takatifu ya nje, sehemu takatifu
ya ndani, pamoja na baraza inayoelekeana
na ukumbi, 16 [n]pamoja na vizingiti,
madirisha membamba na vyumba vyote
vitatu, kila kimoja pamoja na kizingiti
vilifunikwa kwa mbao. Sakafu, ukuta mpaka
kwenye madirisha na madirisha yenyewe
vilifunikwa kwa mbao. 17 Katika nafasi

[a]49 Dhiraa 12 ni sawa na mita 5.4.
[b]**41:1** Zek 6:12; Mt 16:18; Ufu 3:12
[c]1 Dhiraa 6 ni sawa na mita 2.7.
[d]**41:2** 2Nya 3:3
[e]2 Dhiraa 40 ni sawa na mita 18.
[f]3 Dhiraa 7 ni sawa na mita 3.15.
[g]**41:4** 1Fal 6:20; Kut 26:33; Ebr 9:3-8
[h]**41:6** Eze 40:17; 1Fal 6:5-6
[i]**41:7** 1Fal 6:8
[j]**41:8** Isa 28:16; Eze 40:5
[k]12 Dhiraa 90 ni sawa na mita 40.5.
[l]**41:14** Eze 40:47
[m]**41:15** Eze 42:3
[n]**41:16** 1Fal 6:4, 15; Eze 42:3; Isa 54:12; 1Kor 13:12

iliyokuwa juu ya upande wa nje wa ingilio
la sehemu takatifu ya ndani, na katika kuta
zilizozunguka sehemu takatifu ya ndani na
sehemu takatifu ya nje, kwa nafasi zilizo
sawa, 18 [a]kulinakshiwa makerubi na miti
ya mitende. Miti ya mitende ilikuwa kati
ya kerubi na kerubi. Kila kerubi alikuwa
na nyuso mbili: 19 [b]upande mmoja uso wa
mwanadamu kuelekea mti wa mtende na
upande mwingine uso wa simba ukielekea
mti mwingine wa mtende. Ilinakshiwa
kuzunguka Hekalu lote. 20 Kuanzia
sakafu mpaka eneo lililo juu ya ingilio,
palinakshiwa makerubi na miti ya mitende
pamoja na kwenye ukuta wa nje wa
patakatifu.

21 [c]Mahali patakatifu pa nje palikuwa na
miimo ya mlango uliokuwa mraba na ule
uliokuwa katika Patakatifu Pa Patakatifu
ulikuwa unafanana na huo mwingine.
22 [d]Kulikuwa na madhabahu ya mbao kimo
chake dhiraa tatu na ilikuwa dhiraa mbili
mraba pande zote, tako lake na pande zake
zilikuwa za mbao. Yule mtu akaniambia,
"Hii ni meza ambayo iko mbele za Bwana."
23 [e]Mahali patakatifu pa nje na Patakatifu
Pa Patakatifu zilikuwa na milango miwili.
24 [f]Kila mlango ulikuwa na vipande viwili,
vipande viwili vilivyoshikwa na bawaba
vyenye kufunguka kwa kila mlango. 25 Juu
ya hiyo milango ya Patakatifu palinakshiwa
makerubi na miti ya mitende kama yale
yaliyonakshiwa kwenye kuta, na kulikuwa
na ubao ulioning'inia mbele ya baraza
kwa nje. 26 [g]Katika kuta za pembeni za
ukumbi kulikuwa na madirisha membamba
yaliyonakshiwa miti ya mitende kila
upande. Vyumba vya pembeni vya Hekalu
pia vilikuwa vimefunikwa kwa mbao.

*Vyumba Vya Makuhani*

42 [h]Ndipo yule mtu akaniongoza kuelekea
kaskazini mpaka kwenye ua wa
nje na kunileta mpaka kwenye vyumba
vinavyoelekeana na ua wa Hekalu na
kuelekeana na ukuta wa nje upande wa
kaskazini. 2 Jengo ambalo mlango wake
ulielekea kaskazini lilikuwa na urefu wa
dhiraa mia moja na upana wa dhiraa
hamsini. 3 [i]Mbele ya zile dhiraa ishirini
za ule ua wa ndani unaoelekeana na ile
njia ya ua wa nje, kuliinuka vyumba virefu
kimoja baada ya kingine vya ghorofa tatu.
4 [j]Mbele ya hivi vyumba kulikuwa na njia
ya ndani yenye upana wa dhiraa kumi na
urefu wa dhiraa mia moja. Milango yake
ilikuwa upande wa kaskazini. 5 Basi vyumba
vya juu vilikuwa vyembamba zaidi, kwa
kuwa ujia[k] ulichukua nafasi zaidi ndani
yake kuliko katika vyumba vya sakafu ya
chini na vya katikati ya jengo. 6 Vyumba
katika ghorofa ya tatu havikuwa na nguzo,
kama kumbi zilivyokuwa nazo, kwa hiyo
eneo la sakafu ya vyumba vya juu lilikuwa
ni dogo kuliko la sakafu ya chini na ya
kati. 7 Kulikuwa na ukuta wa nje uliokuwa
sambamba na vile vyumba na ukumbi wa
nje, ulitokeza urefu wa dhiraa hamsini.
8 Wakati safu ya vyumba katika ua wa nje
vilikuwa na urefu wa dhiraa hamsini, vile
vyumba vilivyokuwa karibu zaidi na Hekalu
vilikuwa na urefu wa dhiraa mia moja.
9 [l]Vyumba vya chini vilikuwa na ingilio
upande wa mashariki unapoingia kutoka
ukumbi wa nje.

10 [m]Upande wa kusini kufuata urefu wa
ukuta wa ukumbi wa nje, unaopakana
na ukumbi wa Hekalu na kuelekeana
na ukuta wa nje, kulikuwa na vyumba
11 [n]vyenye ujia unayopita mbele yake. Hivi
vilifanana na vile vyumba vya upande wa
kaskazini, vilikuwa na urefu na upana ulio
sawa, mahali pa kutokea na vipimo vyake

---

[a]**41:18** 1Fal 6:18; Kut 37:7; 1Fal 7:36; Eze 10:21; Mwa 3:24; Kut 25:22; 1Fal 2:26
[b]**41:19** Eze 10:14; 1:10
[c]**41:21** Eze 41:1
[d]**41:22** Kut 30:1; 25:23; Mal 1:7-12; Wim 1:12; Eze 23:41
[e]**41:23** 1Fal 6:32
[f]**41:24** 1Fal 6:34
[g]**41:26** Eze 40:16

[h]**42:1** Kut 27:9; Eze 40:17; 41:12-14
[i]**42:3** Eze 41:15-16
[j]**42:4** Eze 46:19
[k]5 *Ujia* ina maana ya njia ndani ya nyumba.
[l]**42:9** Eze 44:5; 46:19
[m]**42:10** Eze 41:12-14; 42:1
[n]**42:11** Eze 42:4

vilikuwa sawa. Kama ilivyokuwa milango ya
upande wa kaskazini, 12 ndivyo ilivyokuwa
milango ya vyumba vya upande wa kusini.
Kulikuwa na ingilio kuanzia mwanzo wa
njia ambao ulikuwa sambamba na ukuta
wa pili uliokuwa upande wa mashariki,
ambako ndiko kwa kuingia vyumbani.
13 [a]Kisha akaniambia, “Vyumba vya
upande wa kaskazini na vya upande wa
kusini ambavyo vinaelekeana na ukumbi
wa Hekalu ni vyumba vya makuhani,
mahali ambapo wale makuhani ambao
humkaribia Bwana watakula zile sadaka
takatifu sana. Huko ndiko watakakoweka
zile sadaka takatifu sana, yaani, sadaka
za nafaka, sadaka za dhambi na sadaka
za hatia, kwa kuwa mahali ni patakatifu.
14 [b]Mara makuhani waingiapo mahali
patakatifu, hawaruhusiwi kwenda kwenye
ukumbi wa nje mpaka wayaache mavazi
ambayo walivaa wakiwa wanahudumu,
kwa kuwa hayo mavazi ni matakatifu.
Inawapasa kuvaa mavazi mengine kabla
hawajakaribia eneo lililo wazi kwa ajili ya
watu.”
15 Alipomaliza kupima vile vilivyokuwa
katika eneo la ndani la Hekalu, akanitoa
nje kupitia lango la upande wa mashariki
na kupima eneo lote linalozunguka:
16 Akapima upande wa mashariki kwa
ule ufito wa kupimia, nao ulikuwa dhiraa
500[c] 17 Akapima upande wa kaskazini,
nao ulikuwa dhiraa 500 kwa ufito ule
wa kupimia. 18 Tena akapima upande wa
kusini, nao ulikuwa dhiraa 500 kwa ufito
ule wa kupimia. 19 Kisha akageukia upande
wa magharibi na kuupima, ulikuwa dhiraa
500 kwa ufito ule wa kupimia. 20 [d]Hivyo
akapima eneo katika pande zote nne.
Lilikuwa na ukuta kulizunguka wenye urefu
wa dhiraa 500 na upana wa dhiraa 500,
uliotenganisha mahali Patakatifu na eneo
la watu wote.

*Utukufu Warudi Hekaluni*

43 [e]Kisha yule mtu akanileta kwenye
lango linaloelekea upande wa
mashariki, 2 [f]nami nikaona utukufu wa
Mungu wa Israeli ukija kutoka upande
wa mashariki. Sauti yake ilikuwa kama
ya ngurumo ya maji yaendayo kasi, nayo
nchi ikang’aa kwa utukufu wake. 3 [g]Maono
niliyoyaona yalikuwa kama maono yale
niliyokuwa nimeyaona wakati Mungu
alipokuja kuangamiza mji na kama maono
niliyokuwa nimeyaona kando ya Mto
wa Kebari, nami nikaanguka kifudifudi.
4 [h]Utukufu wa Bwana ukaingia hekaluni
kwa kupitia lango linaloelekea upande
wa mashariki. 5 [i]Kisha Roho akanichukua
na kunileta katika ule ua wa ndani, nao
utukufu wa Bwana ulilijaza Hekalu.
6 [j]Wakati yule mtu akiwa amesimama
kando yangu, nilisikia mtu mmoja akisema
nami kutoka ndani ya Hekalu. 7 [k]Akasema,
“Mwanadamu, hapa ni mahali pa kiti
changu cha enzi na mahali pa kuweka nyayo
za miguu yangu. Hapa ndipo nitakapoishi
miongoni mwa Waisraeli milele. Kamwe
nyumba ya Israeli hawatalinajisi tena Jina
langu takatifu, yaani, wao wala wafalme
wao, kwa ukahaba wao na kwa sanamu zao
zisizokuwa na uhai za wafalme wao katika
mahali pao pa juu pa kuabudia miungu.
8 [l]Walipoweka kizingiti chao karibu na
kizingiti changu na miimo yao ya milango
karibu na miimo yangu, pakiwa na ukuta tu
kati yangu na wao, walilinajisi Jina langu
takatifu kwa matendo yao ya machukizo.
Kwa sababu hiyo niliwaangamiza kwa
hasira yangu. 9 [m]Basi sasa na waweke mbali

[a]**42:13** Kut 30:20; Eze 40:46; Law 6:29; 14:13; Kut 29:31; Kum 21:5; Hes 18:9-10; Yer 41:5; Eze 41:12-14
[b]**42:14** Law 16:23; Kut 28:40-43; Eze 44:19; Kut 29:9; Law 8:7-9; Kut 29:4-9
[c]16 Dhiraa 500 ni sawa na mita 225.
[d]**42:20** Eze 40:5; Zek 2:5-6; Eze 45:2; Ufu 21:16; Eze 22:26; 43:12
[e]**43:1** Eze 10:19; 1Nya 9:18; Eze 8:16; 42:15
[f]**43:2** Za 18:4; Ufu 1:15; 21:11; Isa 6:3
[g]**43:3** Eze 1:4; 3:21; Yer 1:10
[h]**43:4** Eze 1:28; 10:19; 44:2
[i]**43:5** Eze 3:12; 11:24; Kut 16:7; Isa 6:4
[j]**43:6** Eze 40:3
[k]**43:7** Eze 20:29-39; Law 26:30; Kut 25:8; Yer 16:18; 16:18; 3:17; Eze 37:23
[l]**43:8** 2Fal 16:14
[m]**43:9** Eze 37:26-28

nami ukahaba wao na sanamu za wafalme
wao zisizo na uhai, nami nitakaa miongoni
mwao milele.
10 [a]"Mwanadamu, elezea hilo Hekalu kwa
watu wa Israeli, ili wapate kuona aibu kwa
ajili ya dhambi zao. Wao na wapime hicho
kielelezo. 11 [b]Wakishaona aibu kwa ajili
ya yale yote waliyotenda, wafahamishe
kielelezo cha hilo Hekalu, yaani mpangilio
wake, maingilio yake ya kutoka na kuingia,
kielelezo chake chote, na masharti yake
yote na sheria zake zote. Yaandike haya
mbele yao ili wapate kuwa waaminifu kwa
hicho kielelezo chake na kufuata masharti
yake yote.
12 [c]"Hii ndiyo sheria ya Hekalu: Eneo
lote linalozunguka Hekalu juu ya mlima
litakuwa takatifu kuliko yote. Hii ndiyo
sheria ya Hekalu.

*Madhabahu*

13 [d]"Hivi ndivyo vipimo vya madhabahu
kwa dhiraa ndefu, yaani, dhiraa moja
na nyanda nne:[e] Tako lake liwe na kina
cha hiyo dhiraa moja na upana wa hiyo
dhiraa moja, ikiwa na ukingo wa shibiri
moja[f] kuizunguka pembeni. Hiki kitakuwa
ndicho kimo cha madhabahu: 14 Kimo cha
msingi kuanzia usawa wa ardhi mpaka
kwenye mfereji sehemu ya chini kimo chake
ni dhiraa mbili na upana wake ni dhiraa
moja na kuanzia kwenye ukingo mdogo
hadi kwenye ukingo mpana kimo chake ni
dhiraa nne na upana wake ni dhiraa moja.
15 [g]Pale pawashwapo moto madhabahuni
kimo chake kitakuwa dhiraa nne, na
pembe nne zinazoelekeza juu kutoka pale
pawashwapo moto. 16 [h]Pale pawashwapo
moto pa madhabahu ni mraba, urefu
wake ni dhiraa kumi na mbili[i] na upana
wa dhiraa kumi na mbili. 17 [j]Pia sehemu
ya juu ni mraba, urefu wake dhiraa kumi
na nne na upana wa dhiraa kumi na
nne, ikiwa na ukingo wa nusu dhiraa na
mfereji kuizunguka madhabahu. Ngazi za
kupandia madhabahuni zitaelekea upande
wa mashariki."
18 [k]Kisha akaniambia, "Mwanadamu, hili
ndilo BWANA Mwenyezi asemalo: Haya
ndiyo yatakayokuwa masharti ya kutoa
dhabihu za kuteketezwa na kunyunyiza
damu juu ya madhabahu itakapokuwa
imejengwa. 19 [l]Utatoa fahali mchanga
kuwa sadaka ya dhambi kwa makuhani,
ambao ni Walawi, wa jamaa ya Sadoki, ndio
watakaonikaribia kuhudumu mbele zangu,
asema BWANA Mwenyezi. 20 [m]Itakupasa
kuchukua baadhi ya hiyo damu ya mnyama
huyo na kuiweka juu ya hizo pembe nne
za madhabahu na juu ya ncha zake nne
za sehemu ya juu kuzunguka ukingo
wote, ili kuitakasa madhabahu na kufanya
upatanisho kwa ajili yake. 21 [n]Itakupasa
kumchukua huyo fahali mchanga kwa
ajili ya sadaka ya dhambi na kumteketeza
mahali palipoagizwa katika eneo la Hekalu
nje ya mahali Patakatifu.
22 "Siku ya pili yake utamtoa beberu
asiye na dosari kwa ajili ya sadaka ya
dhambi, nayo madhabahu itatakaswa
kama ilivyotakaswa kwa yule fahali.
23 [o]Utakapokuwa umemaliza kazi ya
kuitakasa, utamtoa fahali mchanga pamoja
na kondoo dume toka kwenye kundi, wote
wawe hawana dosari. 24 [p]Utawatoa mbele
za BWANA, nao makuhani watanyunyizia
chumvi juu yao na kuwatoa kuwa sadaka
ya kuteketezwa kwa BWANA.
25 "Kwa siku saba itakupasa kutoa beberu
kila siku kwa ajili ya sadaka ya dhambi, pia
itakupasa kutoa fahali mchanga na kondoo
dume kutoka zizini, wote wawe hawana

---

[a]**43:10** Eze 16:61; 40:4
[b]**43:11** Eze 44:5-6; Mt 28:20
[c]**43:12** Eze 40:2; 42:20; Ufu 21:27; Eze 17:22
[d]**43:13** Kut 20:24; 2Nya 4:1
[e]13 Dhiraa 1 na nyanda 4 ni sawa na sentimita 53.
[f]13 Shibiri 1 ni sawa na sentimita 22.5.
[g]**43:15** Kut 27:2; Isa 29:2
[h]**43:16** Ufu 21:16
[i]16 Dhiraa 12 ni sawa na mita 5.4.
[j]**43:17** Kut 20:26; Eze 45:19; Kut 27:1
[k]**43:18** Kut 40:29; Ebr 9:21-22
[l]**43:19** Law 4:3; Eze 45:18-19; 2Nya 8:17; Ezr 7:2; Hes 16:40; Eze 40:46
[m]**43:20** Law 16:19; 4:7
[n]**43:21** Kut 29:14; Ebr 13:11
[o]**43:23** Kut 29:1; Law 22:20
[p]**43:24** Mk 9:49-50

dosari. 26 Kwa siku saba itawapasa kufanya
upatanisho kwa ajili ya madhabahu na
kuitakasa na hivyo ndivyo watakavyoiweka
wakfu. 27 [a]Mwishoni mwa hizi siku saba,
kuanzia siku ya nane na kuendelea,
itawapasa makuhani kutoa sadaka zenu
za kuteketezwa na sadaka za amani juu
ya madhabahu. Kisha nitawakubali ninyi,
asema Bwana Mwenyezi.”

*Mkuu, Walawi, Makuhani*

44 [b]Ndipo yule mtu akanirudisha mpaka
kwenye lango la nje la mahali
Patakatifu, lile linaloelekea upande wa
mashariki, nalo lilikuwa limefungwa.
2 [c]Bwana akaniambia, “Lango hili litabaki
limefungwa. Haliruhusiwi kufunguliwa,
wala hakuna mtu yeyote anayeruhusiwa
kuingilia kwenye lango hili. Litabaki
limefungwa kwa sababu Bwana, Mungu
wa Israeli, ameingia kwa kupitia lango
hili. 3 [d]Yeye aliye mkuu peke yake ndiye
anayeweza kukaa penye njia ya hilo lango
na kula chakula mbele za Bwana. Itampasa
aingie kwa njia hiyo ya lango la ukumbini
na kutokea njia iyo hiyo.”

4 [e]Kisha yule mtu akanileta kwa njia ya
lango la kaskazini mpaka mbele ya Hekalu.
Nikatazama nami nikauona utukufu wa
Bwana ukilijaza Hekalu la Bwana, nami
nikaanguka kifudifudi.

5 [f]Bwana akaniambia, “Mwanadamu,
angalia kwa uangalifu, usikilize kwa bidii
na uzingatie kila kitu ninachokuambia
kuhusu masharti yote yanayohusu Hekalu
la Bwana. Uwe mwangalifu kuhusu
wale wanaoruhusiwa hekaluni na wale
wasioruhusiwa kuingia mahali patakatifu.
6 [g]Iambie nyumba ya kuasi ya Israeli,
‘Hili ndilo Bwana Mwenyezi asemalo:
Matendo yenu ya machukizo yatosha, ee
nyumba ya Israeli! 7 [h]Zaidi ya matendo
yenu yote ya machukizo, mmewaleta
wageni wasiotahiriwa mioyo na miili
katika patakatifu pangu, mkilinajisi Hekalu
langu, huku mkinitolea chakula, mafuta
ya wanyama na damu, nanyi mmevunja
Agano langu. 8 [i]Badala ya kutimiza
wajibu wenu kuhusiana na vitu vyangu
vitakatifu, mmeweka watu wengine kuwa
viongozi katika patakatifu pangu. 9 [j]Hili
ndilo Bwana Mwenyezi asemalo: Hakuna
mgeni asiyetahiriwa moyo na mwilini
anayeruhusiwa kuingia patakatifu pangu,
wala hata wageni wanaoishi miongoni mwa
Waisraeli.

10 [k]“ ‘Walawi walioniacha wakati
Waisraeli walipopotoka wakatoka kwangu
na kutangatanga kwa kufuata sanamu
zao, watachukua adhabu ya dhambi zao.
11 [l]Wanaweza wakatumika katika mahali
patakatifu pangu, wakiwa na uangalizi
wa malango ya Hekalu, nao watachinja
sadaka za kuteketezwa na dhabihu kwa
ajili ya watu na kusimama mbele ya watu
ili kuwahudumia. 12 [m]Lakini kwa sababu
waliwatumikia watu mbele ya sanamu
zao na kuifanya nyumba ya Israeli ianguke
kwenye dhambi, kwa hiyo nimeapa kwa
mkono ulioinuliwa kwamba ni lazima
wachukue matokeo ya dhambi yao, asema
Bwana Mwenyezi. 13 [n]Hawaruhusiwi
kukaribia ili kunitumikia kama makuhani
wala kukaribia chochote changu kilicho
kitakatifu au sadaka iliyo takatifu kupita
zote, bali watachukua aibu ya matendo
yao ya kuchukiza. 14 [o]Lakini nitawaweka
katika uangalizi wa Hekalu na kazi zote
zile zinazotakiwa kufanyika ndani yake.

---

[a]**43:27** Kut 32:6; Law 17:5; Ay 42:8; Isa 60:7
[b]**44:1** Eze 43:1
[c]**44:2** Eze 43:4-5
[d]**44:3** Zek 6:12; Kut 24:9-11; Eze 46:2-8
[e]**44:4** Isa 6:4; Ufu 15:8; Eze 1:28; Dan 8:17; Eze 40:35; 10:4
[f]**44:5** Eze 40:4; 43:10-11; 42:9
[g]**44:6** Eze 3:19
[h]**44:7** Law 26:4; Mwa 17:14; Kut 12:48; Mdo 21:28; Law 22:25
[i]**44:8** Law 22:2; Hes 18:7; 2Tim 4:1
[j]**44:9** Yoe 3:17; Zek 14:21
[k]**44:10** Neh 9:34; 2Fal 23:8; Za 95:10; Hes 18:23
[l]**44:11** 2Nya 29:34; Hes 16:9; 1Nya 26:12-19; Hes 3:5-37
[m]**44:12** 2Fal 16:10-16; Yer 14:10; Za 106:26; Yer 18:15
[n]**44:13** Eze 16:6; Hes 18:3; Hos 5:1
[o]**44:14** 1Sam 2:36; 2Fal 23:9; 1Nya 23:28-32

15 [a]“ ‘Lakini makuhani, ambao ni Walawi
na wazao wa Sadoki, ambao walitimiza
wajibu wao kwa uaminifu katika patakatifu
pangu wakati Waisraeli walipopotoka,
watakaribia ili kutumika mbele zangu.
Itawapasa wasimame mbele zangu ili kutoa
dhabihu za mafuta ya wanyama na damu,
asema Bwana Mwenyezi. 16 [b]Wao peke
yao ndio wenye ruhusa ya kuingia mahali
patakatifu pangu. Wao peke yao ndio
watakaokaribia meza yangu ili kuhudumu
mbele zangu na kufanya utumishi wangu.
17 [c]“ ‘Watakapoingia kwenye malango ya
ukumbi wa ndani, watavaa nguo za kitani
safi, hawaruhusiwi kamwe kuvaa mavazi
ya sufu wakati wanapokuwa wakihudumu
kwenye malango ya ukumbi wa ndani wala
ndani ya Hekalu. 18 [d]Watavaa vilemba vya
kitani safi vichwani mwao na nguo za ndani
za kitani safi viunoni mwao. Hawatavaa
chochote kitakachowafanya kutoa jasho.
19 [e]Watakapotoka ili kuingia katika ukumbi
wa nje mahali watu walipo, watavua
nguo walizokuwa wakihudumu nazo na
wataziacha katika vyumba vitakatifu nao
watavaa nguo nyingine, ili kwamba wasije
wakaambukiza watu utakatifu kwa njia ya
mavazi yao.
20 [f]“ ‘Hawatanyoa nywele za vichwa
vyao wala kuziacha ziwe ndefu, bali
watazipunguza. 21 [g]Kuhani yeyote asinywe
mvinyo aingiapo katika ukumbi wa
ndani. 22 [h]Wasioe wanawake wajane wala
walioachika, inawapasa kuoa wanawake
bikira wenye heshima wa Israeli au wajane
wa makuhani. 23 [i]Watawafundisha watu
wangu tofauti kati ya vitu vitakatifu na
vitu vya kawaida na kuwaonyesha jinsi ya
kupambanua kati ya vitu najisi na vitu safi.
24 [j]“ ‘Katika magombano yoyote,
makuhani watatumika kama mahakimu
na kuamua hilo jambo kufuatana na
sheria zangu. Watazishika sheria zangu
na maagizo yangu katika sikukuu zangu
zote zilizoamriwa, nao watatakasa Sabato
zangu.
25 [k]“ ‘Kuhani asijitie unajisi kwa kukaribia
maiti, lakini, kama mtu aliyekufa alikuwa
baba yake au mama yake, mwana au
binti yake, ndugu yake au dada ambaye
hajaolewa, basi aweza kujitia unajisi kwa
hao. 26 [l]Baada ya kujitakasa, atakaa hali
hiyo kwa muda wa siku saba. 27 [m]Siku
atakapoingia katika ukumbi wa ndani
wa mahali patakatifu ili kuhudumu,
atatoa sadaka ya dhambi kwa ajili yake
mwenyewe, asema Bwana Mwenyezi.
28 [n]“ ‘Mimi nitakuwa ndio urithi pekee
walio nao makuhani katika Israeli.
Msiwape wao milki, mimi nitakuwa milki
yao. 29 [o]Wao watakula sadaka za nafaka,
sadaka za dhambi na sadaka za hatia na kila
kitu kitakachotolewa kwa Bwana katika
Israeli kitakuwa chao. 30 [p]Yote yaliyo bora
ya malimbuko ya vitu vyote na matoleo
yenu maalum vitakuwa vya makuhani.
Inawapasa kuwapa malimbuko ya kwanza
ya unga wenu ili kwamba baraka ipate
kuwa katika nyumba zenu. 31 [q]Makuhani
hawaruhusiwi kula chochote, ikiwa ni
ndege au mnyama, aliyekutwa akiwa
amekufa au aliyeraruliwa na wanyama pori.

---

[a]**44:15** Yer 33:18; Zek 3:7; Kum 10:8; 2Sam 8:17; Eze 7:2; Kum 29:13; Eze 40:46
[b]**44:16** Eze 41:22; 1Sam 2:35; Mal 2:7; Law 3:16-17; Hes 8:15; Law 17:5-6
[c]**44:17** Kut 39:27-28; Ufu 19:8
[d]**44:18** Kut 28:39; Isa 3:20; Law 16:4; Kut 28:42
[e]**44:19** Law 6:27; Eze 46:20; Kut 39:27-29; Law 6:10-11
[f]**44:20** Law 21:5; Hes 6:5; Isa 28:7
[g]**44:21** Law 10:9
[h]**44:22** Law 21:7
[i]**44:23** Eze 22:26; Hag 2:11-13; Mal 2:7; Mwa 7:2; Law 13:50; Yer 15:19
[j]**44:24** 1Tim 4:5; 1Nya 23:4; 2Nya 19:8; Kum 17:8-9; 19:17
[k]**44:25** Law 21:1-4
[l]**44:26** Law 21:1-4; Hes 6:10
[m]**44:27** Hes 3:28; 6:11; Law 4:28
[n]**44:28** Kum 10:9; Yos 13:33; Hes 18:20; Kum 18:1-2
[o]**44:29** Law 27:21; Hes 18:9, 14; Yos 13:14; Law 6:16
[p]**44:30** Hes 18:12-13; 2Nya 31:5; Hes 15:18-21; Neh 10:35-37; 2Nya 30:10
[q]**44:31** Kut 22:31; Law 22:8; 11:39-40

*Mgawanyo Wa Nchi*

45 [a]“ ‘Mtakapogawa nchi kuwa urithi,
mtaitoa sehemu ya nchi kwa BWANA
kuwa eneo takatifu, urefu wake dhiraa
25,000,[b] upana wake dhiraa 20,000[c]
eneo hili lote litakuwa takatifu. 2 [d]Katika
hiyo, itakuwepo sehemu mraba ambayo
ni mahali patakatifu kila upande dhiraa
500 ikiwa imezungukwa na eneo la wazi
lenye upana wa dhiraa hamsini. 3 [e]Katika
eneo takatifu, pima sehemu yenye urefu
wa dhiraa 25,000 na upana wa dhiraa
10,000.[f] Ndani ya hilo eneo kutakuwa
mahali patakatifu, Patakatifu pa Patakatifu.
4 [g]Itakuwa sehemu takatifu ya nchi kwa ajili
ya makuhani, wale wanaohudumu ndani
ya mahali patakatifu na ambao hukaribia
ili kuhudumu mbele za BWANA. Patakuwa
mahali pa nyumba zao pamoja na sehemu
kwa ajili ya mahali patakatifu. 5 [h]Eneo
la urefu wa dhiraa 25,000 na upana wa
dhiraa 10,000 litakuwa la Walawi wale
wanaotumika hekaluni, kama milki yao
kwa ajili ya miji ya kuishi.

6 [i]“ ‘Utatoa mji kama mali yao wenye
upana wa dhiraa 5,000[j] na urefu wa dhiraa
25,000, karibu na sehemu takatifu, itakuwa
mali ya nyumba yote ya Israeli.

7 [k]“ ‘Mkuu anayetawala atakuwa na
lile eneo linalopakana na lile eneo
lililowekwa wakfu upande huu na upande
huu na eneo la mji. Eneo la mji litaenea
upande wa magharibi kuanzia upande
wa magharibi na upande wa mashariki
kuanzia upande wa mashariki, likiendelea
kwa urefu kutoka magharibi hadi mpaka
wa mashariki sambamba na mojawapo ya
sehemu za makabila. 8 [l]Nchi hii itakuwa
milki yake katika Israeli. Nao wakuu
wangu hawataonea tena watu wangu bali
watairuhusu nyumba ya Israeli kuimiliki
nchi kulingana na makabila yao.

9 [m]“ ‘Hili ndilo BWANA Mwenyezi asemalo:
Yatosha, enyi wakuu wa Israeli! Acheni
mbali ukatili wenu na uonevu wenu
mkafanye lile lililo haki na sawa. Acheni
kuwatoza watu wangu isivyo haki, asema
BWANA Mwenyezi. 10 [n]Tumieni mizani
sahihi na vipimo sahihi vya efa[o] na bathi.[p]
11 [q]Efa na bathi viwe sawa, bathi iwe sehemu
ya kumi ya homeri na efa iwe sehemu ya
kumi ya homeri, homeri itakuwa ndicho
kiwango cha kukubalika kwa vyote viwili.
12 [r]Shekeli moja itakuwa gera ishirini.[s]
Shekeli ishirini, jumlisha na shekeli ishirini
na tano, jumlisha na shekeli kumi na tano
zitakuwa mina moja.[t]

*Sadaka Na Siku Takatifu*

**(Kutoka 12:1-20; Walawi 23:33-43)**

13 “ ‘Hili ndilo toleo maalum mtakalotoa:
moja ya sita ya efa kutoka kila homeri ya
ngano na moja ya sita ya efa kutoka kila
homeri ya shayiri. 14 Sehemu ya mafuta
iliyoamriwa, yaliyopimwa kwa bathi,
ni sehemu ya kumi ya bathi kutoka kila
kori moja[u] (ambayo ina bathi kumi au
homeri moja.) 15 [v]Pia kondoo mmoja
atachukuliwa kutoka kwenye kila kundi
la kondoo mia mbili kutoka kwenye malisho

[a]**45:1** Mit 3:9-10; Hes 34:13; Eze 47:21-22; 48:8-9, 29
[b]1 Dhiraa 25,000 ni sawa na kilomita 11.25.
[c]1 Dhiraa 20,000 ni sawa na kilomita 9.
[d]**45:2** Eze 42:20
[e]**45:3** Eze 48:10
[f]3 Dhiraa 10,000 ni sawa na kilomita 4.5.
[g]**45:4** Eze 40:46; 48:10-11
[h]**45:5** Eze 48:13; 40:17
[i]**45:6** Eze 48:15-18
[j]6 Dhiraa 5,000 ni sawa na kilomita 2.25.
[k]**45:7** Eze 48:21
[l]**45:8** Hes 26:53; Eze 46:18
[m]**45:9** Yer 22:3; Zek 7:9-10; 8:16; Za 12:5
[n]**45:10** Kum 25:15; Law 19:35; Mit 11:1; Mik 6:10-11; Amo 8:4-6
[o]10 Efa ni kipimo cha ujazo cha kupimia vitu vikavu ambacho ni sawa na omeri 10; efa 1 ni sawa na kilo 22.
[p]10 Bathi ni kipimo cha ujazo cha kupimia vitu vya humiminika ambacho ni sawa na 1/10 ya homeri; homeri 1 ni bathi 10 au efa 10.
[q]**45:11** Isa 5:10
[r]**45:12** Law 27:25; Hes 3:47; Kut 30:13
[s]12 Gera 20 ni sawa na shekeli 1.
[t]12 Mina 1 hapa ni sawa na shekeli 60; mina ya kawaida ilikuwa sawa na shekeli 50.
[u]14 Kori 1 ni sawa na bathi 10 au homeri 1.
[v]**45:15** Law 1:4; 6:30; Rum 5:10; Efe 2:16; Kol 1:21; Tit 2:14

yaliyonyeshewa vizuri ya Israeli. Hivi vitatumika kwa ajili ya sadaka ya nafaka, sadaka ya kuteketezwa na sadaka za amani ili kufanya upatanisho kwa ajili ya watu, asema BWANA Mwenyezi. 16 Watu wote wa nchi wataungana pamoja na mkuu anayetawala Israeli ili kutoa hii sadaka maalum. 17 [a]Huu utakuwa ndio wajibu wa mkuu anayetawala kutoa sadaka ya kuteketezwa, sadaka ya nafaka na sadaka ya kinywaji kwenye sikukuu, Mwezi Mwandamo na Sabato, kwenye sikukuu zote zilizoamriwa za nyumba ya Israeli. Atatoa sadaka za dhambi, sadaka za nafaka, sadaka za kuteketezwa na sadaka za amani ili kufanya upatanisho kwa ajili ya nyumba ya Israeli.

18 [b]“ ‘Hili ndilo BWANA Mwenyezi asemalo: Katika mwezi wa kwanza, siku ya kwanza ya huo mwezi utamchukua fahali mchanga asiye na dosari na kutakasa mahali patakatifu. 19 [c]Kuhani itampasa achukue sehemu ya hiyo damu ya sadaka ya dhambi na kuipaka kwenye miimo ya Hekalu, kwenye pembe nne za juu za ukingo wa hayo madhabahu na juu ya miimo ya lango la ukumbi wa ndani. 20 [d]Itakupasa kufanya vivyo hivyo katika siku ya saba ya mwezi huo kwa ajili ya mtu yeyote ambaye hutenda dhambi bila kukusudia au bila kujua, hivyo utafanya upatanisho kwa ajili ya Hekalu.

21 [e]“ ‘Katika mwezi wa kwanza siku ya kumi na nne utaadhimisha Pasaka. Sikukuu itaendelea kwa siku saba, wakati huo wa hizo siku saba mtakula mikate isiyotiwa chachu. 22 [f]Katika siku hiyo mkuu anayetawala atatoa fahali kuwa sadaka ya dhambi kwa ajili yake mwenyewe na kwa ajili ya watu wote wa nchi. 23 [g]Kila siku wakati wa hizo siku saba za sikukuu atatoa mafahali saba na kondoo dume saba wasio na dosari kuwa sadaka ya kuteketezwa kwa BWANA na beberu kwa ajili ya sadaka ya dhambi. 24 [h]Pia atatoa sadaka ya nafaka efa moja kwa kila fahali na efa moja kwa kila kondoo dume, pamoja na hini moja[i] ya mafuta kwa kila efa.

25 [j]“ ‘Wakati wa hizo siku saba za sikukuu, ambayo huanza katika mwezi wa saba kwenye siku ya kumi na tano, mkuu anayetawala atatoa mahitaji yale yale kwa ajili ya sadaka za dhambi, sadaka za kuteketezwa, sadaka za nafaka na mafuta.

*Sheria Nyingine Mbalimbali*

46 [k]“ ‘Hili ndilo BWANA Mwenyezi asemalo: Lango la ukumbi wa ndani linaloelekea upande wa mashariki litakuwa linafungwa kwa siku sita za juma, ila siku ya Sabato na siku ya Mwezi Mwandamo litafunguliwa. 2 [l]Mkuu anayetawala ataingia kupitia baraza ya njia ya lango la ukumbi na kusimama karibu na nguzo ya lango. Makuhani watatoa sadaka za mkuu anayetawala za kuteketezwa na sadaka za amani. Mkuu anayetawala atasujudu kwenye kizingiti cha njia ya lango, kisha atatoka nje, lakini lango halitafungwa mpaka jioni. 3 [m]Siku za Sabato na za Mwezi mwandamo watu wote wa nchi wataabudu mbele za BWANA penye lile ingilio la ile njia. 4 [n]Sadaka ya kuteketezwa aletazo mkuu anayetawala kwa BWANA siku ya Sabato itakuwa ni wana-kondoo sita na kondoo dume mmoja, wote wasiwe na dosari. 5 [o]Sadaka ya nafaka inayotolewa pamoja na huyo kondoo dume itakuwa efa moja na sadaka ya nafaka inayotolewa na hao wana-kondoo itakuwa kiasi apendacho

[a]**45:17** Yn 6:51; Gal 3:13; Isa 66:23; 1Fal 8:62; 2Nya 31:3; Hes 10:10; Eze 46:4-12
[b]**45:18** Kut 12:2; Law 22:20; Ebr 9:14; Law 16:33
[c]**45:19** Eze 43:17; Law 16:18-19; Eze 43:20
[d]**45:20** Law 4; 27
[e]**45:21** Kut 12:11; Law 23:5-6; Hes 9:2-3
[f]**45:22** Law 4:14; 1Pet 2:24
[g]**45:23** Hes 28:15, 25; 22:40; Ay 42:8
[h]**45:24** Hes 28:12-13; Eze 46:5-7
[i]24 Hini ni kipimo cha kupimia vitu vya humiminika chenye ujazo wa 1/6 ya bathi, na ni sawa na lita 4.
[j]**45:25** Kum 16:13; Law 23:34-43; Hes 29:12-38
[k]**46:1** Eze 40:19; 1Nya 9:18; Isa 66:23
[l]**46:2** Eze 44:3; Mt 25:10; Eze 40:39
[m]**46:3** Za 100:4; Lk 1:10
[n]**46:4** Hes 28:5, 9, 11, 12; Eze 45:17
[o]**46:5** Eze 45:24; Hes 28:12

mtu pamoja na hini ya mafuta kwa kila efa.
6 [a]Siku ya mwezi mwandamo atatoa fahali
mchanga, wana-kondoo sita na kondoo
dume, wote wasiwe na dosari. 7 [b]Atatoa
kuwa sadaka ya nafaka efa moja pamoja
na fahali mmoja, efa moja na kondoo dume
mmoja na pamoja na wana-kondoo kama
atakavyo kutoa, pamoja na hini ya mafuta
kwa kila efa. 8 [c]Wakati mkuu anayetawala
aingiapo, atapitia kwenye baraza ya njia ya
lango, naye atatoka nje kwa njia hiyo hiyo.
9 [d]" 'Wakati watu wa nchi wanapokuja
mbele za BWANA katika sikukuu
zilizoamriwa, yeyote aingiaye kwa lango
la kaskazini kuabudu atatoka nje kwa
lango la kusini na yeyote aingiaye kwa
lango la kusini atatoka nje kwa lango la
kaskazini. Hakuna mtu yeyote atakayerudi
kwa kupitia lango lile aliloingilia, lakini kila
mmoja atatoka nje kwa lango linalokabili
lile aliloingilia. 10 [e]Mkuu anayetawala
atakuwa miongoni mwao, akiingia nao
ndani wanapoingia, naye atatoka nao nje
wanapotoka.
11 [f]" 'Kwenye sikukuu na kwenye sikukuu
zilizoamriwa, sadaka ya nafaka itakuwa
efa moja pamoja na fahali mmoja, efa
moja pamoja na kondoo dume mmoja,
pamoja na idadi ya wana-kondoo kama
mtu apendavyo kutoa, pamoja na hini ya
mafuta kwa kila efa. 12 [g]Mkuu anayetawala
anapotoa sadaka ya hiari kwa BWANA,
ikiwa ni sadaka ya kuteketezwa au sadaka
ya amani, lango linaloelekea mashariki
litafunguliwa kwa ajili yake. Atatoa sadaka
yake ya kuteketezwa au sadaka yake ya
amani kama afanyavyo katika siku ya
Sabato. Kisha atatoka nje, naye akiisha
kutoka nje, lango litafungwa.
13 [h]" 'Kila siku utamtoa mwana-kondoo
wa mwaka mmoja asiyekuwa na dosari kwa
ajili ya sadaka ya kuteketezwa kwa BWANA,
utaitoa kila siku asubuhi. 14 [i]Pia kila siku
asubuhi pamoja na hiyo sadaka utatoa
sadaka ya nafaka, ikiwa na sehemu ya sita
ya efa pamoja na theluthi moja ya hini[j] ya
mafuta ya kuchanganya na ule unga. Utoaji
wa sadaka hii ya nafaka kwa BWANA ni
amri ya daima. 15 [k]Kwa hiyo mwana-kondoo
na sadaka ya nafaka na mafuta vitatolewa
kila siku asubuhi kwa ajili ya sadaka ya
daima ya kuteketezwa.
16 [l]" 'Hili ndilo BWANA Mwenyezi
asemalo: Ikiwa mkuu atawalaye atatoa
zawadi kutoka kwenye urithi wake na
kumpa mmoja wa wanawe, hiyo zawadi
itakuwa pia kwa wazao wake, itakuwa
mali yao kwa urithi. 17 [m]Hata hivyo, kama
atatoa zawadi kutoka urithi wake na kumpa
mmoja wa watumishi wake, mtumishi
anaweza kuiweka mpaka mwaka wa uhuru,
kisha itarudishwa kwa mkuu anayetawala.
Urithi wake ni wa wanawe peke yao, ni
mali yao. 18 [n]Mkuu anayetawala hana
ruhusa kuchukua urithi wowote wa watu
na kuwaondoa kwenye mali zao. Mkuu
atawalaye atawapa wanawe urithi wao,
kutoka kwenye mali zake mwenyewe, ili
kwamba pasiwe na mtu wangu yeyote
atakayetengwa na urithi wake.' "
19 [o]Kisha mtu yule akanileta kwa kupitia
kwenye ingilio lililokuwa kando ya
lango mpaka kwenye vyumba vitakatifu
vinavyoelekea kaskazini, ambavyo ni vya
makuhani, naye akanionyesha mahali
fulani upande wa mwisho wa magharibi.
20 [p]Akaniambia, "Mahali hapa ndipo
makuhani watakapotokosea sadaka ya hatia
na sadaka ya dhambi na kuoka sadaka ya
nafaka, kuepuka kuzileta katika ukumbi wa
nje na kushirikisha utakatifu kwa watu."
21 Baada ya hapo akanileta kwenye

---

[a]**46:6** Hes 10:10; Law 22:20
[b]**46:7** Eze 45:24
[c]**46:8** Eze 46:2
[d]**46:9** Kut 23:14; 34:20; Kum 16:16
[e]**46:10** 2Sam 6:14-15; Za 42:4
[f]**46:11** Eze 46:5
[g]**46:12** Eze 45:17; Gal 2:20; Yn 10:18; Law 7:16
[h]**46:13** Kut 29:28; Hes 28:3; Za 5:3
[i]**46:14** Dan 8:11; Hes 15:6
[j]14 Theluthi moja ya hini ni sawa na lita 1.3.
[k]**46:15** Kut 29:38-42; Hes 28:5-6
[l]**46:16** 2Nya 21:3
[m]**46:17** Law 25:9-10; Isa 61:2
[n]**46:18** Law 25:23; Mik 2:1-2; Za 78:72; Isa 8:14; Eze 45:8
[o]**46:19** Eze 42:4-9
[p]**46:20** Law 6:27; Zek 14:20; Law 2:4-7

ukumbi wa nje na kunizungusha kwenye
pembe zake nne, nami nikaona katika
kila pembe ya huo ukumbi kulikuwa na
ukumbi mwingine. 22 Katika pembe nne
za huo ukumbi wa nje kulikuwa na kumbi
nyingine, zenye urefu wa dhiraa arobaini na
upana wake dhiraa thelathini, ambapo hizo
kumbi kwenye hizo pembe nne zilikuwa na
vipimo vilivyo sawa. 23 Mzunguko wa ndani
wa hizo kumbi nne ulikuwa na ukingo
wa jiwe, zikiwa na sehemu zilizojengwa
kwa ajili ya moto kuzunguka chini ya huo
ukingo. 24 [a]Akaniambia, "Hizi ndizo sehemu
za kupikia ambazo wale wanaohudumu
kwenye Hekalu watatokosea dhabihu za
watu."

*Mto Kutoka Hekaluni*

47 [b]Yule mtu akanirudisha mpaka kwenye
ingilio la Hekalu, nami nikaona maji
yakitoka chini ya kizingiti cha Hekalu
yakitiririkia upande wa mashariki (kwa
maana upande wa mbele wa Hekalu
ulielekea mashariki). Maji yalikuwa
yakitoka chini upande wa kusini wa
Hekalu, kusini mwa madhabahu. 2 [c]Ndipo
akanitoa nje kupitia lango la kaskazini na
kunizungusha mpaka kwenye lango la nje
linaloelekea mashariki, nayo maji yalikuwa
yakitiririka kutoka upande wa kusini.

3 [d]Mtu yule alipokwenda upande wa
mashariki akiwa na kamba ya kupimia
mkononi mwake, akapima dhiraa 1,000[e]
kisha akanipitisha kwenye hayo maji
ambayo yalifika kwenye vifundo vya
miguu. 4 Akapima dhiraa 1,000 nyingine
na kunipitisha kwenye hayo maji ambayo
yalifika magotini. Akapima dhiraa nyingine
1,000 na kunipitisha kwenye hayo maji
ambayo yalifika kiunoni. 5 [f]Akapima tena
dhiraa 1,000 nyingine, lakini wakati huu
yalikuwa mto ambao sikuweza kuvuka,
kwa kuwa maji yalikuwa na kina kirefu
ambacho ni cha kuogelea, mto ambao
hakuna mtu yeyote ambaye angeweza
kuvuka. 6 [g]Akaniuliza, "Je, mwanadamu,
unaona hili?"

Kisha akanirudisha mpaka kwenye
ukingo wa huo mto. 7 [h]Nilipofika pale,
nikaona idadi kubwa ya miti kila upande
wa ule mto.

8 [i]Akaniambia, "Haya maji yanatiririka
kuelekea nchi ya mashariki na kushuka
mpaka Araba,[j] ambapo huingia Baharini.
Yanapomwagikia kwenye hiyo Bahari,[k] maji
yaliyoko humo huponywa na kuwa safi.
9 [l]Popote mto huu uendapo kila kiumbe hai
kinachoyaparamia hayo maji kitaishi, nako
kutakuwa na samaki wengi mno, mara maji
haya yafikapo huko. Maji hayo yatakuwa
hai na kila kitu kitakachoishi kule mto
uendako. 10 [m]Wavuvi watasimama kando
ya bahari, kuanzia En-Gedi hadi En-Eglaimu
huko patakuwa mahali pa kutandaza nyavu
za kuvulia samaki. Samaki watakuwa wa
aina nyingi, kama samaki wa Bahari Kuu[n]
11 [o]Lakini madimbwi yake na mabwawa
yake hayatakuwa na maji yanayofaa
kunywa, bali yatabakia kuwa maji ya
chumvi. 12 [p]Miti ya matunda ya kila aina
itaota kwenye kingo zote mbili za mto huu.
Majani yake hayatanyauka wala haitaacha
kuwa na matunda katika matawi yake. Kila
mwezi kutakuwa na matunda, kwa sababu
maji yatokayo patakatifu yanaitiririkia.
Matunda yake yatakuwa chakula na majani
yake yatakuwa dawa."

---

[a]**46:24** Eze 46:20; Rum 12:1; 15:16; Ebr 13:16
[b]**47:1** Za 46:4; Ufu 22:1; Yoe 3:18; Isa 55:1
[c]**47:2** Eze 40:35
[d]**47:3** Eze 40:3; Ufu 11:1
[e]3 Dhiraa 1,000 ni sawa na mita 450.
[f]**47:5** Isa 11:9; Hab 2:14; Mwa 2:10
[g]**47:6** Ufu 22:2; Isa 41:19
[h]**47:7** Eze 47:12; Ufu 22:2; Za 1:3; 92:12
[i]**47:8** Ufu 17:15; Yos 3:16; Isa 41:18; Kum 3:17
[j]8 Araba hapa ina maana ya Bonde la Yordani.
[k]8 Bahari hapa ina maana ya Bahari ya Chumvi.
[l]**47:9** Isa 12:3; Yn 4:14; 1Kor 15:45; Yn 7:37-38
[m]**47:10** Isa 19:8; Mt 4:19; Yos 15:62; Eze 26:5; Mt 13:47; Hes 34:6
[n]10 Bahari Kuu hapa ina maana ya Bahari ya Mediterania.
[o]**47:11** Kum 29:23
[p]**47:12** Mwa 2:9; Ufu 22:2; Yer 17:8; Ay 18:6; Eze 36:8

*Mipaka Mipya Ya Nchi*

13 [a]Hili ndilo BWANA Mwenyezi asemalo: "Hii ndiyo mipaka ambayo kwayo mtagawanya hiyo nchi kuwa urithi miongoni mwa hayo makabila kumi na mawili ya Israeli, pamoja na mafungu mawili ya Yosefu.
14 [b]Mtagawa kwa usawa miongoni mwao. Kwa sababu niliapa kwa mkono ulioinuliwa kuwapa baba zenu, nchi hii itakuwa urithi wenu.

15 [c]"Huu ndio utakuwa mpaka wa hiyo nchi:

"Upande wa kaskazini utaanzia
Bahari Kuu kwa njia ya Hethloni
kupitia Lebo-Hamathi hadi
maingilio ya Sedadi.
16 [d]Berotha
na Sibraimu (ambao uko kwenye
mpaka kati ya Dameski na
Hamathi), hadi kufikia Haser-Hatikoni, ambao uko katika mpaka
wa Haurani.
17 [e]Hivyo mpaka
utaendelea kuanzia Baharini hadi
Hasar-Enoni, ukiambaa na mpaka
wa kaskazini wa Dameski, pamoja
na mpaka wa Hamathi upande
wa kaskazini. Huu utakuwa ndio
mpaka wa kaskazini.
18 [f]Upande wa mashariki mpaka
utapita kati ya Haurani na
Dameski, kuambaa Yordani na kati
ya Gileadi na nchi ya Israeli, hadi
bahari ya mashariki[g] na kufika
Tamari. Huu utakuwa ndio mpaka
wa mashariki.
19 [h]Upande wa kusini utaanzia Tamari
hadi kufikia maji ya Meriba-Kadeshi, kisha utaambaa na Kijito
cha Misri hadi Bahari Kuu. Huu
utakuwa ndio mpaka wa kusini.
20 [i]Upande wa magharibi, Bahari
Kuu itakuwa ndio mpaka hadi
kwenye sehemu mkabala na
Lebo-Hamathi. Huu utakuwa ndio
mpaka wa magharibi.

21 [j]"Mtagawanya nchi hii miongoni mwenu kufuatana na makabila ya Israeli.
22 [k]Mtaigawanya kuwa urithi kwa ajili yenu na kwa ajili ya wageni wanaoishi miongoni mwenu na ambao wana watoto. Wao watakuwa kwenu kama wenyeji wazawa wa Israeli, pamoja na ninyi watagawiwa urithi miongoni mwa makabila ya Israeli.
23 [l]Katika kabila lolote mgeni atakapoishi hapo ndipo mtakapompatia urithi wake," asema BWANA Mwenyezi.

*Mgawanyo Wa Nchi*

48 [m]"Haya ndiyo majina ya makabila na sehemu zao: Kwenye mpaka wa kaskazini, Dani atakuwa na sehemu moja, mpaka huo utafuata barabara ya Hethloni hadi Lebo-Hamathi, Hasar-Enani hata mpaka wa kaskazini wa Dameski karibu na Hamathi utakuwa sehemu ya huo mpaka wake kuanzia upande wa mashariki hadi upande wa magharibi.
2 [n]"Asheri atakuwa na sehemu moja, itapakana na nchi ya Dani kuanzia mashariki hadi upande wa magharibi.
3 [o]"Naftali atakuwa na sehemu moja, itapakana na nchi ya Asheri kuanzia mashariki hadi magharibi.
4 [p]"Manase atakuwa na sehemu moja, itapakana na nchi ya Naftali kuanzia mashariki hadi magharibi.
5 [q]"Efraimu atakuwa na sehemu moja,

[a]**47:13** Hes 34:2-12; Yer 3:18; Mwa 48:5-16; 49:26
[b]**47:14** Kum 1:8; Mwa 12:7; Eze 36:12
[c]**47:15** Eze 48:1; Hes 34:2-8
[d]**47:16** 2Sam 8:8; Hes 13:21; Yer 49:23; Amo 6:2
[e]**47:17** Hes 34:9; Eze 48:1
[f]**47:18** Eze 27:18
[g]18 Bahari ya mashariki hapa ina maana ya Bahari ya Chumvi.
[h]**47:19** Mwa 15:18; Kum 32:51; Isa 27:12; Eze 48:28
[i]**47:20** Hes 13:21; 34:6; Eze 48:1
[j]**47:21** Kum 24:19; Efe 2:19-22; Rum 10:12; Law 24:22; Mal 3:5; Efe 3:6; Isa 56:6-7
[k]**47:22** Mdo 2:5; Efe 2:19-22; Rum 10:12; Efe 3:6; Ufu 7:9-10; Gal 3:28; Kol 3:11
[l]**47:23** Kum 10:19
[m]**48:1** Mwa 30:6; Hes 34:7-9; Eze 47:15-20
[n]**48:2** Yos 19:24-31
[o]**48:3** Yos 19:32-39
[p]**48:4** Yos 17:1-11
[q]**48:5** Yos 16:5-9; 17:7-10, 17

itapakana na nchi ya Manase kuanzia
mashariki hadi magharibi.
6 [a]“Reubeni atakuwa na sehemu moja,
itapakana na nchi ya Efraimu kuanzia
mashariki hadi magharibi.
7 [b]“Yuda atakuwa na sehemu moja,
itapakana na nchi ya Reubeni kuanzia
mashariki hadi magharibi.
8 [c]“Kupakana na nchi ya Yuda kuanzia
mashariki mpaka magharibi itakuwa ndiyo
sehemu utakayoitoa ili kuwa toleo maalum.
Itakuwa na upana wa dhiraa 25,000[d] na
urefu wake kuanzia mashariki mpaka
magharibi utakuwa ule ule wa sehemu
moja ya kabila, mahali patakatifu patakuwa
katikati ya eneo hilo.
9 [e]“Hiyo sehemu maalum mtakayotoa
kwa BWANA itakuwa na urefu wa dhiraa
25,000 na upana wa dhiraa 10,000[f] 10 [g]Hii
itakuwa ni sehemu takatifu kwa ajili ya
makuhani. Itakuwa na urefu wa dhiraa
25,000 upande wa kaskazini, upana wa
dhiraa 10,000 upande wa magharibi,
dhiraa 10,000 upande wa mashariki
na urefu wa dhiraa 25,000 upande wa
kusini. Katikati yake patakuwa mahali
patakatifu pa BWANA. 11 [h]Hii itakuwa kwa
ajili ya makuhani waliowekwa wakfu,
Wasadoki, waliokuwa waaminifu katika
kunitumikia nao hawakupotoka kama
Walawi walivyofanya wakati Waisraeli
walipopotoka. 12 Itakuwa toleo maalum
kwao kutoka sehemu takatifu ya nchi,
yaani, sehemu takatifu sana, inayopakana
na nchi ya Walawi.
13 [i]“Kando ya nchi ya makuhani, Walawi
watakuwa na mgawo wa urefu wa dhiraa
25,000 na upana wa dhiraa 10,000. Urefu
wake utakuwa jumla dhiraa 25,000 na upana
wa dhiraa 10,000. 14 [j]Hawataruhusiwa
kuuza wala kuibadilisha hata mojawapo.
Hii ndiyo sehemu nzuri ya nchi kuliko
nyingine zote, hivyo haitakuwa mikononi
mwa watu wengine, kwa sababu ni takatifu
kwa BWANA.
15 [k]“Eneo linalobaki lenye upana wa
dhiraa 5,000[l] na urefu wa dhiraa 25,000,
litakuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida
ya mji, kwa ajili ya ujenzi wa nyumba
na malisho. Mji utakuwa katikati yake
16 [m]nao utakuwa na vipimo hivi: upande
wa kaskazini dhiraa 4,500,[n] upande wa
kusini dhiraa 4,500, upande wa mashariki
dhiraa 4,500 na upande wa magharibi
dhiraa 4,500. 17 Sehemu ya malisho kwa
ajili ya mji itakuwa na eneo la dhiraa 250[o]
upande wa kaskazini, dhiraa 250 upande
wa kusini, dhiraa 250 upande wa mashariki
na dhiraa 250 upande wa magharibi.
18 [p]Eneo linalobaki, linalopakana na sehemu
takatifu likiwa na urefu sawa nalo, litakuwa
dhiraa 10,000 upande wa mashariki na
dhiraa 10,000 upande wa magharibi.
Mazao yake yatawapa watumishi wa mji
chakula. 19 [q]Watumishi wa mji wanaolima
shamba hili watatoka katika makabila yote
ya Israeli. 20 [r]Eneo lote la hiyo sehemu
litakuwa mraba, yaani, dhiraa 25,000 kila
upande. Kama toleo maalum mtatenga
sehemu takatifu, pamoja na milki ya mji.
21 [s]“Eneo linalobaki pande zote za eneo
linalofanya sehemu takatifu na milki ya mji
litakuwa mali ya mkuu atawalaye. Eneo
hili litaenea upande wa mashariki kuanzia
kwenye dhiraa 25,000 za sehemu takatifu
hadi mpaka wa mashariki na kuelekea
upande wa magharibi kuanzia kwenye
dhiraa 25,000 hadi mpaka wa magharibi.

[a]**48:6** Yos 13:15-21
[b]**48:7** Yos 15:1-63
[c]**48:8** Eze 45:1; 48:21
[d]8 Dhiraa 25,000 ni sawa na kilomita 11.25.
[e]**48:9** Eze 45:1
[f]9 Dhiraa 10,000 ni sawa na kilomita 4.5.
[g]**48:10** Eze 45:1-4
[h]**48:11** 2Sam 8:17; Law 8:35; Eze 14:11; 44:15; Yer 23:11; Neh 9:34
[i]**48:13** Eze 45:5
[j]**48:14** Law 25:34; 27:10, 28
[k]**48:15** Kum 20:5; Eze 42:20; 44:23; 45:6
[l]15 Dhiraa 5,000 ni sawa na kilomita 2.25.
[m]**48:16** Ufu 21:16
[n]16 Dhiraa 4,500 ni sawa na kilomita 2.025.
[o]17 Dhiraa 250 ni sawa na sentimita 112.5.
[p]**48:18** Eze 21:16
[q]**48:19** Eze 45:6; Ufu 7:5
[r]**48:20** Hes 24:5; Isa 33:20; Ufu 21:16
[s]**48:21** Eze 45:7; Yos 18:1; Yn 12:32; Rum 15:9-12

Maeneo yote haya mawili yanayoenda
sambamba na urefu wa sehemu za makabila
yatakuwa ya mkuu anayetawala, na sehemu
ile takatifu pamoja na mahali patakatifu
pa Hekalu itakuwa katikati yake. [22] Kwa
hiyo milki ya Walawi na milki ya mji
vitakuwa katikati ya eneo lile ambalo ni
mali ya mkuu anayetawala. Eneo la mkuu
anayetawala litakuwa kati ya mpaka wa
Yuda na mpaka wa Benyamini.

[23] [a]“Kuhusu makabila yaliyobaki:
Benyamini atakuwa na sehemu moja,
itakayoanzia upande wa mashariki hadi
upande wa magharibi.

[24] [b]“Simeoni atakuwa na sehemu moja,
itakayopakana na nchi ya Benyamini
kuanzia mashariki hadi magharibi.

[25] [c]“Isakari atakuwa na sehemu moja,
itakayopakana na nchi ya Simeoni kuanzia
mashariki hadi magharibi.

[26] [d]“Zabuloni atakuwa na sehemu moja,
itakayopakana na nchi ya Isakari kuanzia
mashariki hadi magharibi.

[27] [e]“Gadi atakuwa na sehemu moja,
itakayopakana na nchi ya Zabuloni kuanzia
mashariki hadi magharibi.

[28] [f]“Mpaka wa kusini wa Gadi utapita
kusini kuanzia Tamari hadi maji ya Meriba-
Kadeshi, kisha kupitia upande wa Kijito cha
Misri hadi Bahari Kuu.[g]

[29] [h]“Hii ndiyo nchi mtakayogawanya
kuwa urithi kwa makabila ya Israeli, nazo
zitakuwa sehemu zao,” asema Bwana
Mwenyezi.

*Malango Ya Mji*

[30] “Haya yatakuwa ndiyo malango ya mji
ya kutokea: Kuanzia upande wa kaskazini,
ambayo urefu wake ni dhiraa 4,500,
utakuwa na malango matatu, [31] [i]malango
hayo ya mji yatapewa majina ya makabila
ya Israeli. Malango hayo matatu ya upande
wa kaskazini moja litakuwa lango la
Reubeni, lango la Yuda na lango la Lawi.

[32] “Upande wa mashariki, wenye urefu
wa dhiraa 4,500, utakuwa na malango
matatu: lango la Yosefu, lango la Benyamini
na lango la Dani.

[33] “Upande wa kusini, wenye urefu wa
dhiraa 4,500, utakuwa na malango matatu:
lango la Simeoni, lango la Isakari na lango
la Zabuloni.

[34] [j]“Upande wa magharibi, wenye urefu
wa dhiraa 4,500, utakuwa na malango
matatu: lango la Gadi, lango la Asheri na
lango la Naftali.

[35] [k]“Urefu wote kuzunguka utakuwa
dhiraa 18,000.[l]

“Nalo jina la mji huo kuanzia wakati huo
na kuendelea litakuwa:

Bwana yupo hapa.”

[a]**48:23** Yos 18:11-28
[b]**48:24** Mwa 29:33; Yos 19:1-9
[c]**48:25** Yos 19:17-23
[d]**48:26** Yos 13:24-28
[e]**48:27** Yos 13:24-28
[f]**48:28** Mwa 14:7; Hes 34:6, 15; Mwa 15:18; Isa 27:12; Eze 47:19
[g]28 Bahari Kuu hapa ina maana ya Bahari ya Mediterania.
[h]**48:29** Eze 47:14, 21, 22; 45:1
[i]**48:31** Ufu 21:12; Isa 60:18
[j]**48:34** 2Nya 4:4; Ufu 21:12-13
[k]**48:35** Za 72:8; Ufu 21:3; Zek 2:10; Amu 6:24; Isa 12:6; 24:23; Yer 31:17
[l]35 Dhiraa 18,000 ni sawa na kilomita 8.1.

# DANIELI

*Mafunzo Ya Danieli Huko Babeli*

1 [a]Katika mwaka wa tatu wa utawala
wa Yehoyakimu mfalme wa Yuda,
Nebukadneza mfalme wa Babeli alikuja
akazingira Yerusalemu kwa jeshi. 2 [b]Bwana
akamtia Yehoyakimu mfalme wa Yuda
mkononi mwa Nebukadneza, pamoja na
baadhi ya vyombo kutoka Hekalu la Mungu.
Hivi akavichukua hadi kwenye hekalu la
mungu wake huko Shinari, naye akaviweka
nyumbani ya hazina ya mungu wake.
3 [c]Kisha mfalme akamwagiza Ashpenazi,
mkuu wa maafisa wa mfalme, kumletea
baadhi ya Waisraeli kutoka jamaa ya
mfalme na kutoka jamaa kuu, 4 vijana
wanaume wasio na dosari mwilini, wenye
sura nzuri, wanaoonyesha kipaji katika
kila aina ya elimu, wenye ufahamu
mzuri, wepesi kuelewa, na waliofuzu
kuhudumu katika jumba la kifalme.
Alikuwa awafundishe lugha na maandiko
ya Wakaldayo. 5 [d]Mfalme akawaagizia kiasi
cha chakula na divai ya kila siku kutoka
meza ya mfalme. Walikuwa wafundishwe
kwa miaka mitatu, na hatimaye waingie
kwenye utumishi wa mfalme.
6 [e]Baadhi ya hawa vijana walitoka Yuda:
nao ni Danieli, Hanania, Mishaeli na Azaria.
7 [f]Mkuu wa maafisa akawapa majina mapya:
Danieli akamwita Belteshaza, Hanania
akamwita Shadraki, Mishaeli akamwita
Meshaki, na Azaria akamwita Abednego.
8 [g]Lakini Danieli alikusudia kuwa hatajitia
unajisi kwa chakula cha mfalme na divai,
naye akamwomba mkuu wa maafisa ruhusa
ili asijinajisi kwa njia hii. 9 [h]Basi Mungu
alikuwa amemfanya huyo mkuu wa maafisa
kuonyesha upendeleo na huruma kwa
Danieli, 10 [i]lakini huyo mkuu wa maafisa
akamwambia Danieli, "Ninamwogopa
bwana wangu mfalme, aliyeagizia chakula
na kinywaji chenu. Kwa nini aone nyuso
zenu zikiwa mbaya kuliko za vijana
wengine wa rika lenu? Mfalme atakata
kichwa changu kwa sababu yenu."
11 Ndipo Danieli akamwambia mlinzi
aliyeteuliwa na huyo mkuu wa maafisa
kuwasimamia Danieli, Hanania, Mishaeli na
Azaria, 12 [j]"Tafadhali wajaribu watumishi
wako kwa siku kumi. Usitupe chochote ila
nafaka na mboga za majani[k] tule, na maji ya
kunywa. 13 Baadaye ulinganishe sura zetu
na vijana wanaokula chakula cha mfalme,
ukawatendee watumishi wako kulingana
na unachoona." 14 [l]Basi akakubali jambo
hili, akawajaribu kwa siku kumi.
15 [m]Mwisho wa zile siku kumi,
walionekana kuwa na afya na kunawiri
zaidi kuliko yeyote kati ya wale vijana
waliokula chakula cha mfalme. 16 Hivyo
mlinzi wao akaondoa chakula chao na
divai yao waliopangiwa kula na kunywa,
akawapa nafaka na mboga za majani badala
yake.
17 [n]Mungu akawapa hawa vijana wanne
maarifa na ufahamu wa kila aina ya
maandiko na elimu. Naye Danieli aliweza
kufahamu maono na aina zote za ndoto.
18 Mwisho wa muda uliowekwa na mfalme
kuwaingiza kwake, mkuu wa maafisa

[a]**1:1** Yer 28:4; 35:11; 46:2; 2Nya 36:6; 2Fal 24:1
[b]**1:2** 2Nya 36:7; Yer 27:19; Zek 5:5-11; 2Fal 24:13
[c]**1:3** 2Fal 20:18; Isa 39:7; Amu 8:18; Mdo 7:20-22; Mwa 39:6; Ezr 4:7
[d]**1:5** Es 2:5-6, 9
[e]**1:6** Eze 14:14; Dan 2:17-25
[f]**1:7** Dan 5:12; 10:1; Isa 39:7; Dan 3:12; 2:49; 2:26
[g]**1:8** Mwa 39:21; Mit 16:7; 1Fal 8:50; Eze 4:13-14
[h]**1:9** Mwa 39:21; Mit 16:7; 1Fal 8:50
[i]**1:10** Ufu 2:10
[j]**1:12** Ufu 2:10
[k]12 Nafaka na mboga za majani, yaani *zeroimu* kwa Kiebrania, ina maana ya aina za ngano na shayiri, na jamii ya kunde kama maharagwe, dengu, choroko, n.k.
[l]**1:14** Mhu 2:26; Yak 1:5; Dan 2:19, 30; 7:1; 8:1
[m]**1:15** Kut 23:25
[n]**1:17** 1Fal 3:12; Ay 12:13; Mhu 2:26; Dan 2:23; Kol 1:9; Dan 5:11; Mdo 7:22

akawaleta mbele ya Mfalme Nebukadneza. [19] [a]Mfalme akazungumza nao, akaona hakuna aliyelingana na Danieli, Hanania, Mishaeli na Azaria. Hivyo wakaingia katika utumishi wa mfalme. [20] [b]Katika kila jambo la hekima na ufahamu kuhusu kile mfalme alichowauliza, aliwaona bora mara kumi zaidi kuliko waganga na wasihiri wote katika ufalme wake wote.

[21] [c]Naye Danieli akabaki huko mpaka mwaka wa kwanza wa utawala wa Mfalme Koreshi.

*Ndoto Ya Nebukadneza*

2 [d]Katika mwaka wa pili wa utawala wake, Nebukadneza aliota ndoto. Mawazo yake yakasumbuka na hakuweza kulala. [2] [e]Hivyo mfalme akawaita waganga, wasihiri, wachawi na wanajimu ili wamwambie ndoto yake aliyokuwa ameota. Walipoingia ndani na kusimama mbele ya mfalme, [3] [f]akawaambia, "Niliota ndoto inayonisumbua, nami nataka nijue maana yake."

[4] [g]Ndipo wanajimu wakamjibu mfalme kwa lugha ya Kiaramu,[h] "Ee mfalme, uishi milele! Waambie watumishi wako hiyo ndoto, nasi tutaifasiri."

[5] [i]Mfalme akawajibu wanajimu, "Nimeamua hivi kwa uthabiti: Ikiwa hamtaniambia ndoto yangu ilikuwa ipi na kuifasiri, mtakatwa vipande vipande na nyumba zenu zitafanywa kuwa vifusi. [6] [j]Lakini mkiniambia ndoto yangu na kuielezea, mtapokea kwangu zawadi, tuzo na heshima kubwa. Basi niambieni ndoto yangu na mnifasirie."

[7] Wakajibu kwa mara nyingine, "Mfalme na awaambie watumishi wake ndoto yake, nasi tutaifasiri."

[8] Ndipo mfalme akajibu, "Nina hakika kuwa mnajaribu kupata muda zaidi, kwa sababu mnatambua kuwa nimeamua hivi kwa uthabiti: [9] [k]Ikiwa hamtaniambia ndoto yangu, ipo adhabu moja tu kwenu. Mmefanya shauri kuniambia habari za kunipotosha na mambo maovu, mkitumaini kwamba hali itabadilika. Hivyo basi, niambieni hiyo ndoto, nami nitajua kuwa mwaweza kunifasiria."

[10] [l]Wanajimu wakamjibu mfalme, "Hakuna mtu duniani ambaye anaweza kufanya analotaka mfalme! Vilevile hakuna mfalme hata awe mkuu na mwenye uweza namna gani, aliyeuliza kitu kama hicho kwa mganga au kwa msihiri, wala kwa mnajimu yeyote. [11] [m]Anachouliza mfalme ni kigumu mno. Hakuna yeyote awezaye kumfunulia mfalme isipokuwa miungu, nao hawaishi miongoni mwa wanadamu."

[12] [n]Jambo hili lilimkasirisha na kumghadhibisha mfalme mno hata kuagiza kuuawa kwa wenye hekima wote wa Babeli. [13] [o]Hivyo amri ikatolewa ya kuwaua wenye hekima, nao watu wakatumwa kuwatafuta Danieli na rafiki zake ili wawaue.

[14] Wakati Arioko, mkuu wa askari wa walinzi wa mfalme, alikuwa amekwenda kuwaua watu wenye hekima wa Babeli, Danieli akazungumza naye kwa hekima na busara. [15] Akamuuliza huyo afisa wa mfalme, "Kwa nini mfalme ametoa amri kali hivyo?" Ndipo Arioko akamweleza Danieli jambo hilo. [16] Aliposikia jambo hili, Danieli akamwendea mfalme, akamwomba ampe muda ili aweze kumfasiria ile ndoto.

[17] Ndipo Danieli akarudi nyumbani kwake na kuwaeleza rafiki zake Hanania, Mishaeli na Azaria jambo hilo. [18] [p]Aliwasihi waombe rehema kutoka kwa Mungu wa

[a]**1:19** Mwa 41:46
[b]**1:20** Es 2:15; Eze 28:3; Mwa 41:8; 1Fal 4:30; Dan 4:18; 2:13; 6:3
[c]**1:21** Dan 6:28; 2Nya 36:22; Dan 10:1
[d]**2:1** Mwa 20:3; 41:8; Ay 33:15-18; Es 6:1; Dan 6:18; 4:5
[e]**2:2** Mwa 41:8; Kut 7:11; Yer 27:9; Isa 9:13; 44:25; Dan 4:6
[f]**2:3** Dan 4:5
[g]**2:4** Ezr 4:7; Neh 2:3; Dan 5:10
[h]4 Kutoka hapa hadi Dan 7:28, mwandishi aliandika na Kiaramu.
[i]**2:5** Ezr 6:11; Dan 3:29; Mwa 41:32
[j]**2:6** Dan 5:7, 16
[k]**2:9** Es 4:11; Isa 41:22-24; 2:10
[l]**2:10** Dan 3:8; 4:7; 5:8
[m]**2:11** Kut 8:10; Mwa 41:38; Dan 5:11
[n]**2:12** Dan 3:13-19; Mit 16:14; 28:15
[o]**2:13** Dan 1:20; 5:19
[p]**2:18** Isa 37:4; Yer 33:3; Ufu 11:13; Ezr 1:2; Neh 1:4

mbinguni kuhusu siri hii, ili yeye na rafiki
zake wasije wakauawa pamoja na wenye
hekima wengine wa Babeli. 19 [a]Wakati wa
usiku lile fumbo lilifunuliwa kwa Danieli
katika maono. Ndipo Danieli akamhimidi
Mungu wa mbinguni, 20 [b]na akasema:

“Lihimidiwe jina la Mungu milele na
milele;
hekima na uweza ni vyake.
21 [c]Yeye hubadili nyakati na majira;
huwaweka wafalme na
kuwaondoa.
Huwapa hekima wenye hekima,
na maarifa wenye ufahamu.
22 [d]Hufunua siri na mambo
yaliyofichika;
anajua yale yaliyo gizani,
nayo nuru hukaa kwake.
23 [e]Ninakushukuru na kukuhimidi,
Ee Mungu wa baba zangu:
Umenipa hekima na uwezo,
umenijulisha kile tulichokuomba,
umetujulisha ndoto ya mfalme.”

*Danieli Aifasiri Ndoto*

24 [f]Ndipo Danieli akamwendea Arioko,
ambaye mfalme alikuwa amemteua kuwaua
wenye hekima wa Babeli, akamwambia,
“Usiwaue wenye hekima wa Babeli.
Nipeleke kwa mfalme, nami nitamfasiria
ndoto yake.”
25 [g]Arioko akampeleka Danieli kwa
mfalme mara moja na kumwambia,
“Nimempata mtu miongoni mwa watu wa
uhamisho kutoka Yuda ambaye anaweza
kumwambia mfalme maana ya ndoto yake.”
26 [h]Mfalme akamuuliza Danieli (aliyeitwa
pia Belteshaza), “Je, unaweza kuniambia
nilichoona katika ndoto yangu na kuifasiri?”
27 [i]Danieli akajibu, “Hakuna mwenye
hekima, msihiri, mganga au mwaguzi
anayeweza kumweleza mfalme siri
aliyouliza, 28 [j]lakini yuko Mungu mbinguni
afunuaye siri. Amemwonyesha Mfalme
Nebukadneza kitakachotokea siku zijazo.
Ndoto yako na maono yaliyopita mawazoni
mwako ulipokuwa umelala kitandani
mwako ni haya:
29 “Ee mfalme, ulipokuwa umelala
kitandani, yalikujia mawazo kuhusu
mambo yatakayotokea baadaye, naye
mfunuaji wa siri akakuonyesha ni kitu
gani kitakachotokea. 30 [k]Kwangu mimi,
nimefunuliwa siri hii, si kwa sababu
nina hekima kubwa kuliko watu wengine
wanaoishi, bali ni ili wewe, ee mfalme,
upate kujua tafsiri, na ili uweze kuelewa
kile kilichopita mawazoni mwako.
31 [l]“Ee mfalme, ulitazama, na mbele
yako ilisimama sanamu kubwa, kubwa
mno kupita kiasi, sanamu iliyong’aa na
kutisha kwa kuonekana kwake. 32 Kichwa
cha ile sanamu kilikuwa kimetengenezwa
kwa dhahabu safi, kifua chake na mikono
yake vilikuwa vya fedha, tumbo lake na
mapaja yake vilikuwa vya shaba, 33 miguu
yake ilikuwa ya chuma, na nyayo zake
zilikuwa chuma nazo sehemu nyingine
zilikuwa udongo wa mfinyanzi uliochomwa.
34 [m]Ulipokuwa unaangalia, jiwe lilikatwa,
lakini si kwa mikono ya mwanadamu. Lile
jiwe liliipiga ile sanamu kwenye nyayo
zake za chuma na udongo wa mfinyanzi, na
kuivunja. 35 [n]Ndipo ile chuma, ule udongo
wa mfinyanzi, ile shaba, ile fedha na ile
dhahabu vikavunjika vipande vipande kwa
wakati mmoja, na vikawa kama makapi

[a]**2:19** Ay 33:15; Dan 1:17; Hes 12:6; Yos 22:23
[b]**2:20** Za 113:2; 145:1-2; Ay 9:4; Yer 32:19; Ay 12:13
[c]**2:21** Dan 7:25; Ay 12:19; Rum 13:1; Yak 1:5; Yer 27:5; Za 75:6-7; 2Sam 14:17; Dan 4:17
[d]**2:22** Mwa 40:8; 1Kor 2:10; Ay 12:22; Ebr 4:13; Isa 45:7; Yak 1:17; Za 139:11-12; Dan 4:17
[e]**2:23** Mwa 31:5; Kut 3:15; Dan 1:17; Eze 28:3
[f]**2:24** Eze 28:3
[g]**2:25** Dan 5:13; 6:13; Kum 21:10; Dan 1:6
[h]**2:26** Dan 1:7
[i]**2:27** Mwa 41:8
[j]**2:28** Yer 10:7; Amo 4:13; Dan 4:5; Mwa 40:8; Dan 10:14; Mt 24:6; Eze 28:3; Dan 1:20
[k]**2:30** Mwa 41:16; Mdo 3:12; Isa 45:3; Amo 4:13; Dan 1:7
[l]**2:31** Isa 25:3-5; Hab 1:7
[m]**2:34** Ay 12:19; Zek 4:6; Isa 60:12; Dan 8:25; Ay 34:24; Za 2:9
[n]**2:35** Isa 41:15-16; 2:3; Ufu 11:15; Za 37:10; Isa 17:13; Zek 12:3; Za 1:4

katika sakafu ya kupuria nafaka wakati wa
kiangazi. Upepo ukavipeperusha bila kuacha
hata alama. Lakini lile jiwe lililoipiga ile
sanamu likawa mlima mkubwa mno na
kuijaza dunia yote.
36 [a]“Hii ndiyo iliyokuwa ndoto, nasi sasa
tutamfasiria mfalme. 37 [b]Ee mfalme, wewe ni
mfalme wa wafalme. Mungu wa mbinguni
amekupa wewe utawala, uweza, nguvu na
utukufu. 38 [c]Mikononi mwako amewaweka
wanadamu, wanyama wa kondeni, na ndege
wa angani. Popote waishipo amekufanya
wewe kuwa mtawala juu yao wote. Wewe
ndiye kile kichwa cha dhahabu.
39 [d]“Baada yako, ufalme mwingine
utainuka, ulio dhaifu kuliko wako.
Baadaye utafuata ufalme wa tatu, ule wa
shaba, nao utatawala juu ya dunia yote.
40 [ef]Hatimaye, kutakuwako na ufalme wa
nne, wenye nguvu kama chuma, kwa
maana chuma huvunja na kupondaponda
kila kitu; kama vile chuma ivunjavyo
vitu vipande vipande, ndivyo ufalme huo
utakavyopondaponda na kuvunjavunja
nyingine zote. 41 Kama vile ulivyoona kuwa
kwa sehemu nyayo na vidole vilikuwa
vya udongo wa mfinyanzi uliochomwa na
kwa sehemu nyingine chuma, hivyo huu
utakuwa ufalme uliogawanyika; hata hivyo
utakuwa na sehemu zenye nguvu za chuma
ndani yake, kama vile ulivyoona chuma
imechanganywa na udongo wa mfinyanzi.
42 Kama vile vidole vyake vya miguu
vilikuwa kwa sehemu chuma na sehemu
udongo wa mfinyanzi, hivyo ufalme huo
kwa sehemu utakuwa na nguvu na kwa
sehemu udhaifu. 43 Kama vile ulivyoona
chuma kikiwa kimechanganyikana na
udongo wa mfinyanzi uliochomwa, ndivyo
watu watakavyokuwa mchanganyiko, wala
hawatabaki wameungana tena, kama vile
chuma kisivyoweza kuchanganyikana na
udongo wa mfinyanzi.
44 [g]“Katika siku za wafalme hao, Mungu
wa mbinguni atauweka ufalme ambao
kamwe hautaangamizwa, wala hautaachiwa
taifa jingine. Utaziponda zile falme zote
na kuzikomesha, bali wenyewe utadumu
milele. 45 [h]Hii ndiyo maana ya maono ya
jiwe lililochongwa kutoka mlimani, lakini
si kwa mikono ya mwanadamu, lile jiwe
ambalo lilivunja chuma, shaba, udongo
wa mfinyanzi, fedha na dhahabu vipande
vipande.
“Mungu Mkuu amemwonyesha mfalme
kile kitakachotokea wakati ujao. Ndoto hii
ni ya kweli na tafsiri yake ni ya kuaminika.”
46 [i]Ndipo Mfalme Nebukadneza
akaanguka kifudifudi mbele ya Danieli
kumpa heshima, akaagiza wamtolee Danieli
sadaka na uvumba. 47 [j]Mfalme akamwambia
Danieli, “Hakika Mungu wako ni Mungu
wa miungu, na Bwana wa wafalme, na
mfunuaji wa siri zote, kwa maana umeweza
kufunua siri hii.”
48 [k]Ndipo mfalme akamweka Danieli
nafasi ya juu, na kumpa zawadi nyingi tele.
Akamfanya kuwa mtawala wa jimbo lote la
Babeli, na kumweka kuwa mkuu wa wenye
hekima wote. 49 [l]Zaidi ya hayo, kwa ombi
la Danieli, mfalme akawateua Shadraki,
Meshaki na Abednego kuwa wasimamizi
wa jimbo la Babeli, huku Danieli akibaki
katika ukumbi wa mfalme.

### *Sanamu Ya Dhahabu Na Moto Mkali*

3 [m]Mfalme Nebukadneza alitengeneza
sanamu ya dhahabu, yenye kimo

[a]**2:36** Mwa 40:12
[b]**2:37** Ezr 7:12; Eze 26:7; Yer 27:7; Dan 4:26
[c]**2:38** Dan 4:21; Yer 27:6; Dan 5:18
[d]**2:39** Dan 7:5
[e]**2:40** Dan 7:7; Yn 11:48; Dan 7:23
[f]**2:40** Ufu 12:3; Eze 40:2; Dan 8:7-10
[g]**2:44** Mwa 27:29; Mt 21:43-44; 1Sam 9:20; Isa 60:12; Ufu 11:15; 1Kor 15:24-25; Za 145:13; Isa 9:7; Dan 4:34; 6:26; 7:14, 27; Oba 1:12; Mik 4:7, 13; Lk 1:33
[h]**2:45** Isa 28:16; Dan 8:25; Mwa 41:25; Ufu 22:6
[i]**2:46** Mdo 10:25; Dan 8:17; Mdo 14:13; Ezr 6:10
[j]**2:47** Kum 10:17; Dan 11:36; 4:25; 1Tim 6:15; Dan 4:25; 4:9
[k]**2:48** Es 8:2; Dan 8:27; Mwa 41:40; 2Fal 25:28; Dan 1:20; 4:9; 5:11
[l]**2:49** Dan 3:30; Mit 28:12; 1:7; Es 2:19; Amo 5:15; Dan 6:2; 3:30
[m]**3:1** Isa 41:24; 46:6; Hab 2:19; Yer 16:20

cha dhiraa sitini,[a] na upana wa dhiraa
sita,[b] akaisimamisha kwenye tambarare
ya Dura katika jimbo la nchi ya Babeli.
2 [c]Kisha mfalme akaita wakuu, wasimamizi,
watawala, washauri, watunza hazina,
waamuzi, mahakimu na maafisa wengine
wote wa jimbo kuja kuizindua sanamu
ambayo Mfalme Nebukadneza alikuwa
ameisimamisha. 3 [d]Basi wakuu, wasimamizi,
watawala, washauri, watunza hazina,
waamuzi, mahakimu na maafisa wengine
wa jimbo walikusanyika ili kuizindua
sanamu ile Mfalme Nebukadneza alikuwa
ameisimamisha, nao wakasimama mbele
ya hiyo sanamu.

4 [e]Ndipo mpiga mbiu akatangaza kwa
sauti kubwa, "Enyi watu wa kabila zote,
mataifa na watu wa kila lugha, hili
ndilo mnaloamriwa kulifanya: 5 [f]Mara
mtakaposikia sauti ya baragumu, filimbi,
marimba, zeze, kinubi, zumari na aina
zote za sauti za ala za uimbaji, lazima
mwanguke chini na kuabudu sanamu ya
dhahabu ambayo Mfalme Nebukadneza
ameisimamisha. 6 [g]Mtu yeyote ambaye
hataanguka chini na kuiabudu sanamu
hiyo, atatupwa saa iyo hiyo ndani ya tanuru
iwakayo moto."

7 Kwa hiyo, mara waliposikia sauti ya
baragumu, filimbi, kinubi, zeze, kinanda
na aina zote za ala za uimbaji, watu wa
kabila zote, mataifa na watu wa kila lugha
wakaanguka chini na kuiabudu ile sanamu
ya dhahabu ambayo Mfalme Nebukadneza
alikuwa ameisimamisha.

8 [h]Wakati huo baadhi ya Wakaldayo
walijitokeza na kuwashtaki Wayahudi.
9 [i]Wakamwambia Mfalme Nebukadneza,
"Ee mfalme, uishi milele! 10 [j]Ee mfalme,
umetoa amri kwamba kila mmoja
atakayesikia sauti ya baragumu, filimbi,
kinubi, zeze, kinanda, zumari na aina zote
za ala za uimbaji lazima aanguke chini na
kuiabudu ile sanamu ya dhahabu, 11 na
kwamba yeyote ambaye hataanguka chini
na kuiabudu atatupwa saa iyo hiyo ndani
ya tanuru iwakayo moto. 12 [k]Lakini wako
baadhi ya Wayahudi ambao umewaweka
juu ya mambo ya jimbo la Babeli: yaani,
Shadraki, Meshaki na Abednego, ambao
hawakujali wewe, ee mfalme. Hawaitumikii
miungu yako wala kuiabudu ile sanamu ya
dhahabu uliyoisimamisha."

13 [l]Mfalme Nebukadneza, akiwa
amekasirika na mwenye ghadhabu kali,
akawaita Shadraki, Meshaki na Abednego.
Hivyo watu hawa wakaletwa mbele ya
mfalme, 14 [m]naye Nebukadneza akawauliza,
"Je, ni kweli kwamba ninyi Shadraki,
Meshaki na Abednego hamuitumikii
miungu yangu wala kuiabudu sanamu ya
dhahabu niliyoisimamisha? 15 [n]Basi wakati
mtakaposikia sauti ya baragumu, filimbi,
marimba, zeze, kinubi, zumari na aina
zote za ala za uimbaji, kama mtakuwa
tayari kusujudu na kuiabudu hiyo sanamu
niliyoitengeneza, vyema sana. Lakini kama
hamtaiabudu, mtatupwa saa iyo hiyo ndani
ya tanuru iwakayo moto. Naye ni mungu
yupi atakayeweza kuwaokoa ninyi, kutoka
mkono wangu?"

16 [o]Shadraki, Meshaki na Abednego
wakamjibu mfalme, "Ee Nebukadneza,
hatuhitaji kujitetea mbele zako kuhusu
jambo hili. 17 [p]Ikiwa tutatupwa ndani
ya tanuru iwakayo moto, Mungu
tunayemtumikia anaweza kutuokoa na
moto, naye atatuokoa kutoka mkononi
mwako, ee mfalme. 18 [q]Lakini hata ikiwa
hatatuokoa, ee mfalme, tunataka ufahamu

[a]1 Dhiraa sitini ni sawa na mita 27.
[b]1 Dhiraa sita ni sawa na mita 2.7.
[c]**3:2** Es 1:1; Dan 6:7
[d]**3:3** Rum 1:20-23; Mdo 19:34-35; Mt 7:13
[e]**3:4** Dan 6:25; Ufu 10:11; Dan 4:1
[f]**3:5** Dan 4:1
[g]**3:6** Yer 29:22; Ufu 13:15; Mt 13:42, 50; Dan 5:19; 6:7
[h]**3:8** Isa 19:3; Dan 2:10; Ezr 4:12-16
[i]**3:9** Neh 2:3; Dan 6:6; Hos 7:3
[j]**3:10** Dan 6:12
[k]**3:12** Dan 2:49; 6:13; Es 3:3
[l]**3:13** Dan 2:12; Mdo 5:25-27; Mk 13:9
[m]**3:14** Isa 46:1; Yer 50:2
[n]**3:15** Isa 36:18-20; Kut 5:22; 2Nya 32:15; 32:15; Kut 5:22
[o]**3:16** Mt 10:18-19; Dan 1:7
[p]**3:17** Mwa 48:16; Za 18:48; Ay 5:19; 2Kor 1:10; Dan 6:20; Yer 1:8
[q]**3:18** Kut 1:17; Yos 24:15

kwamba, hatutaitumikia miungu yako
wala kuiabudu sanamu ya dhahabu
uliyoisimamisha."
19 [a]Ndipo Nebukadneza akawa na
ghadhabu kali sana kwa Shadraki, Meshaki
na Abednego, nayo nia yake ikabadilika
kwao. Akaagiza tanuru ichochewe moto
mara saba kuliko kawaida yake 20 na
kuwaamuru baadhi ya askari wake wenye
nguvu zaidi katika jeshi lake kuwafunga
Shadraki, Meshaki na Abednego na
kuwatupa ndani ya tanuru iwakayo moto.
21 Hivyo watu hawa, walifungwa na
kutupwa ndani ya tanuru iwakayo moto
wakiwa wamevaa majoho yao, suruali,
vilemba na nguo zao nyingine. 22 Amri ya
mfalme ilikuwa ya haraka sana na tanuru
ilikuwa na moto mkali kiasi kwamba miali
ya moto iliwaua wale askari waliowapeleka
Shadraki, Meshaki na Abednego. 23 Watu
hawa watatu walianguka ndani ya tanuru
iwakayo moto wakiwa wamefungwa kwa
uthabiti sana.
24 Ndipo Mfalme Nebukadneza
akashangaa, akainuka kwa haraka na
kuwauliza washauri wake, "Je, hawakuwa
watu watatu ambao tuliwafunga na
kuwatupa ndani ya moto?"
Washauri wakajibu, "Hakika, ee mfalme."
25 Mfalme akasema, "Tazama! Naona
watu wanne wakitembeatembea ndani ya
moto, hawajafungwa wala kudhurika, naye
mtu yule wa nne anaonekana kama mwana
wa miungu."
26 Ndipo Nebukadneza akaukaribia
mdomo wa ile tanuru iwakayo moto
na kupaza sauti, "Shadraki, Meshaki na
Abednego, watumishi wa Mungu Aliye Juu
Sana, tokeni! Njooni hapa!"
Ndipo Shadraki, Meshaki na Abednego
wakatoka ndani ya moto. 27 [b]Nao maliwali,
wasimamizi, watawala na washauri wa
mfalme wakakusanyika kuwazunguka.
Waliona kwamba moto haukudhuru
miili yao, wala unywele wa vichwa vyao
haukuungua, majoho yao hayakuungua,
wala hapakuwepo na harufu ya moto
kwenye miili yao.
28 [c]Ndipo Nebukadneza akasema,
"Ahimidiwe Mungu wa Shadraki, Meshaki
na Abednego, ambaye amemtuma
malaika wake na kuwaokoa watumishi
wake. Walimtumaini na kukaidi amri ya
mfalme, nao wakawa tayari kufa kuliko
kutumikia au kuabudu mungu mwingine
yeyote isipokuwa Mungu wao. 29 [d]Kwa hiyo
ninaamuru kwamba watu wa taifa lolote au
lugha yoyote watakaosema kitu chochote
dhidi ya Mungu wa Shadraki, Meshaki
na Abednego wakatwe vipande vipande
na nyumba zao zifanywe kuwa malundo
ya kokoto, kwa maana hakuna mungu
mwingine awezaye kuokoa namna hii."
30 [e]Kisha mfalme akawapandisha vyeo
Shadraki, Meshaki na Abednego katika
jimbo la Babeli.

*Ndoto Ya Nebukadneza Ya Mti*

4 [f]Mfalme Nebukadneza,

Kwa kabila za watu, mataifa na
watu wa kila lugha, wanaoishi katika
ulimwengu wote:

Mafanikio yawe kwenu sana!

2 [g]Ni furaha yangu kuwaambia
kuhusu ishara za miujiza na maajabu
ambayo Mungu Aliye Juu Sana
amenifanyia.

3 [h]Ishara zake ni kuu aje,
na maajabu yake yana nguvu aje!
Ufalme wake ni ufalme wa milele;
enzi yake hudumu kutoka kizazi
hadi kizazi.

4 [i]Mimi, Nebukadneza, nilikuwa
nyumbani katika jumba langu la
kifalme, nikiwa ninaishi kwa raha

[a]**3:19** Law 26:18-28
[b]**3:27** Dan 6:7; Ebr 11:32-34; Za 91:3-11; Dan 6:23; Isa 43:2
[c]**3:28** Za 34:7; Mdo 5:19; Kum 31:20; Ay 13:15; Dan 6:22; Za 97:10; Mdo 12:11
[d]**3:29** Dan 6:26-27; Ezr 6:11
[e]**3:30** Dan 2:49
[f]**4:1** Dan 3:4; 6:25
[g]**4:2** Dan 3:26; Za 74:9
[h]**4:3** Za 105:27; Dan 6:25-27; 2:44
[i]**4:4** Za 30:6; Isa 32:9

na hali ya kufanikiwa. 5 [a]Niliota
ndoto iliyoniogopesha. Nilipokuwa
nimelala kitandani mwangu, njozi
na maono yaliyopita mawazoni
mwangu vilinitisha. 6 [b]Hivyo nikaagiza
kwamba watu wote wenye hekima
wa Babeli waletwe mbele yangu
kunifasiria ndoto yangu. 7 [c]Walipokuja
waganga, wasihiri, wanajimu na
waaguzi, niliwaambia ndoto yangu,
lakini hawakuweza kunifasiria.
8 [d]Mwishoni, Danieli alikuja mbele
yangu nikamweleza hiyo ndoto.
(Danieli anaitwa Belteshaza, kwa jina
la mungu wangu, nayo roho ya miungu
mitakatifu inakaa ndani yake.)

9 [e]Nilisema, “Belteshaza, mkuu wa
waganga, ninajua kuwa roho ya miungu
mitakatifu iko ndani yako, wala hakuna
siri iliyo ngumu kwako. Hii ndiyo
ndoto yangu, nifasirie. 10 [f]Haya ndiyo
maono niliyoona nilipokuwa nimelala
kitandani mwangu: Nilitazama, na
mbele yangu ulisimama mti katikati
ya nchi. Ulikuwa mrefu sana. 11 [g]Mti
ule ulikua, ukawa mkubwa na wenye
nguvu, nayo ncha yake ikagusa anga;
ulionekana mpaka miisho ya dunia.
12 [h]Majani yake yalikuwa ya kupendeza,
matunda yake yalikuwa mengi, na juu
yake kulikuwa na chakula kwa ajili ya
wote. Chini ya kivuli chake wanyama
wa kondeni walipata hifadhi, na ndege
wa angani waliishi katika matawi yake.
Kila kiumbe kililishwa kutokana na mti
huo.

13 [i]“Katika maono niliyoyaona
nikiwa nimelala kitandani mwangu,
nilitazama, na mbele yangu alikuwepo
mlinzi, aliye mtakatifu, akishuka
kutoka mbinguni. 14 [j]Akaita kwa sauti
kubwa: ‘Kateni mti huu, myafyeke
matawi yake; yaondoeni majani
yake na kuyatawanya matunda yake.
Wanyama na wakimbie kutoka chini
yake na ndege waondoke kutoka
matawi yake. 15 Lakini acheni kisiki
chake na mizizi, kikiwa kimefungwa
kwa chuma na shaba, kibaki ardhini,
kwenye majani ya kondeni.

“ ‘Mwacheni aloweshwe na umande
wa mbinguni, naye aachwe aishi
pamoja na wanyama miongoni mwa
mimea ya dunia. 16 Akili yake na
ibadilishwe kutoka ile ya mwanadamu
na apewe akili ya mnyama, mpaka
nyakati saba zipite juu yake.

17 [k]“ ‘Uamuzi huu umetangazwa na
walinzi, hukumu imetangazwa na
watakatifu, ili walio hai wajue kuwa
Aliye Juu Sana ndiye anayetawala
juu ya falme zote za wanadamu, naye
humpa yeyote amtakaye na kumtawaza
juu yake hata yeye aliye mnyonge sana
miongoni mwa wanadamu.’

18 [l]“Hii ndiyo ndoto niliyoipata
mimi, Mfalme Nebukadneza. Sasa
Belteshaza, niambie maana yake,
kwa maana hakuna hata mmoja wa
wenye hekima katika ufalme wangu
anayeweza kunifasiria. Bali wewe
waweza, kwa sababu roho ya miungu
mitakatifu imo ndani yako.”

*Danieli Anafasiri Ndoto*

19 [m]Ndipo Danieli (aliyeitwa pia
Belteshaza) alipofadhaika sana
kwa muda, nayo mawazo yake
yakamtia hofu. Basi mfalme akasema,
“Belteshaza, usiruhusu ndoto wala
maana yake kukutia hofu.”

Belteshaza akamjibu, “Bwana
wangu, laiti ndoto hii ingehusu adui

---

[a]**4:5** Dan 2:1, 28; Za 4:4; Mwa 41:8; Ay 3:26; Dan 5:6; 2:3
[b]**4:6** Dan 2:2
[c]**4:7** Mwa 41:8; Isa 44:25; Dan 2:2, 10
[d]**4:8** Mwa 41:38; Dan 5:11-14; 1:7
[e]**4:9** Dan 2:48; 5:11-12
[f]**4:10** Za 4:4; Eze 31:3-4
[g]**4:11** Eze 19:11; 31:5
[h]**4:12** Eze 17:23; Mt 13:32; Mao 4:20
[i]**4:13** Dan 8:13; Kum 33:2; Dan 7:1
[j]**4:14** Mt 3:10; Dan 5:20; Ay 24:20; Eze 31:2
[k]**4:17** Za 83:18; Rum 13:1; Mt 23:12; Dan 11:21; Za 83:18; Yer 27:5-7; Za 103:19
[l]**4:18** Mwa 41:8; Dan 5:8, 15; 1:20; Mwa 41:38; Dan 1:20
[m]**4:19** Mwa 41:15; Dan 10:16-17; 2Sam 18:32; Mwa 41:8; 40:12; Dan 7:15, 28; 8:27

zako, na maana yake iwahusu watesi
wako! [20] Mti uliouona, uliokua ukawa
mkubwa na wenye nguvu, nayo ncha
yake ikagusa anga na kuonekana
duniani kote, [21] [a]ukiwa na majani ya
kupendeza na matunda mengi, ukitoa
chakula kwa wote, na ukiwapa hifadhi
wanyama wa kondeni na kuwa mahali
pa viota katika matawi yake kwa ajili
ya ndege wa angani. [22] [b]Ee mfalme,
wewe ndiwe ule mti! Umekuwa
mkubwa na mwenye nguvu, nao
ukuu wako umekua mpaka kufika juu
angani, nayo mamlaka yako yameenea
mpaka miisho ya dunia.

[23] [c]"Ee mfalme, wewe ulimwona
mlinzi, aliye mtakatifu, akishuka
kutoka mbinguni na kusema, 'Ukateni
mti na kuuangamiza, lakini kiacheni
kisiki kikiwa kimefungwa kwa chuma
na kwa shaba, kwenye majani ya
kondeni, wakati mizizi yake inabaki
ardhini. Mwacheni aloweshwe na
umande wa mbinguni, mwacheni aishi
kama wanyama pori mpaka nyakati
saba zipite juu yake.'

[24] [d]"Ee mfalme, hii ndiyo tafsiri,
na hii ni amri ya Aliye Juu Sana
aliyoitoa dhidi ya bwana wangu
mfalme: [25] [e]Wewe utafukuzwa mbali
na wanadamu, nawe utaishi pamoja na
wanyama pori; utakula manyasi kama
ng'ombe, na kuloana kwa umande wa
mbinguni. Nyakati saba zitapita juu
yako, mpaka utakapokubali kuwa Yeye
Aliye Juu Sana ndiye anayetawala
juu ya falme za wanadamu, naye
humtawaza yeyote amtakaye. [26] [f]Amri
ya kuacha kisiki pamoja na mizizi yake
inamaanisha kwamba ufalme wako
utarejezwa kwako utakapokubali
kwamba Mbingu ndizo zitawalazo.
[27] [g]Kwa hiyo, ee mfalme, uwe radhi
kupokea shauri langu: Acha dhambi
zako kwa kutenda yaliyo haki, ukaache
uovu wako, na uwe na huruma kwa
walioonewa. Hivyo itawezekana baada
ya hayo, mafanikio yako yakaendelea."

*Ndoto Inatimia*

[28] [h]Haya yote yalimpata Mfalme
Nebukadneza. [29] Miezi kumi na miwili
baadaye, mfalme alipokuwa akitembea
juu ya paa la jumba la kifalme la Babeli,
[30] [i]alisema, "Je, huu si Babeli mji mkuu
nilioujenga kama makao ya kifalme,
kwa uwezo wangu mkubwa, na kwa
ajili ya utukufu wa enzi yangu?"

[31] [j]Maneno hayo yalikuwa bado
katika midomo yake wakati sauti
ilipokuja kutoka mbinguni, ikisema,
"Mfalme Nebukadneza, hiki ndicho
kilichoamriwa kwa ajili yako: Mamlaka
yako ya ufalme yameondolewa
kutoka kwako. [32] [k]Utafukuzwa mbali
na wanadamu, ukaishi pamoja na
wanyama pori, na utakula manyasi
kama ng'ombe. Nyakati saba zitapita
juu yako, mpaka utakapokubali kuwa
Yeye Aliye Juu Sana ndiye anayetawala
juu ya falme za wanadamu, naye
humtawaza yeyote amtakaye."

[33] [l]Papo hapo yale yaliyokuwa
yamesemwa kuhusu Nebukadneza
yakatimia. Alifukuzwa mbali na
wanadamu, akala majani kama
ng'ombe. Mwili wake ulilowesha kwa
umande wa mbinguni mpaka nywele
zake zikakua kama manyoya ya tai na
kucha zake kama makucha ya ndege.

---

[a]**4:21** Eze 31:6
[b]**4:22** 2Sam 12:7; Yer 27:7; Dan 2:37-38; Ay 20:5; Dan 5:18-19
[c]**4:23** Dan 8:13; 5:21; Eze 31:3-4
[d]**4:24** Ay 40:12; Yer 40:2; Ay 34:19; Isa 46:10-11; Za 107:40
[e]**4:25** Za 83:18; Yer 27:5; Dan 2:47; Ay 24:8; Dan 5:21; Za 83:18
[f]**4:26** Dan 2:37; Lk 15:18
[g]**4:27** Isa 55:6-7; Kum 24:13; 1Fal 21:29; Mdo 8:22; Za 41:3; Mit 28:13; Yer 29:7; Eze 18:22
[h]**4:28** Hes 23:19; 2Sam 22:28; Dan 5:20
[i]**4:30** Mit 16:18; Isa 37:24-25; Hab 1:11; Isa 13:19; 10:13; Dan 5:20
[j]**4:31** 2Sam 22:28; Dan 5:20
[k]**4:32** Ay 9:12
[l]**4:33** Ay 20:5; Dan 5:20-21; Ay 24:8

34 [a]Mwisho wa huo wakati, mimi
Nebukadneza, niliinua macho yangu
kuelekea mbinguni, nazo fahamu
zangu zikanirudia. Ndipo nikamsifu
Yeye Aliye Juu Sana, nikamheshimu
na kumhimidi yeye aishiye milele.

Utawala wake ni utawala wa milele;
ufalme wake hudumu kutoka
kizazi na kizazi.
35 [b]Mataifa yote ya dunia
yanahesabiwa kuwa si kitu.
Hufanya kama atakavyo
kwa majeshi ya mbinguni,
na kwa mataifa ya dunia.
Hakuna anayeweza kuuzuia mkono
wake
au kumwambia, "Umefanya nini
wewe?"

36 [c]Wakati huo huo fahamu zangu
ziliponirudia, nikarudishiwa heshima
yangu na fahari yangu kwa ajili ya
utukufu wa ufalme wangu. Washauri
wangu na wakuu wangu walikuja
kunitafuta, nami nikarudishwa kwenye
kiti changu cha ufalme hata nikawa
mkuu kuliko mwanzoni. 37 [d]Basi
mimi, Nebukadneza, humhimidi,
na humtukuza na kumsifu Mfalme
wa mbinguni, kwa sababu kila kitu
afanyacho ni haki, na njia zake zote
ni adili. Nao waendao kwa kiburi
anaweza kuwashusha.

### *Maandishi Ukutani*

5 [e]Mfalme Belshaza alifanya karamu kubwa
kwa ajili ya maelfu ya wakuu wake na
akanywa mvinyo pamoja nao. 2 [f]Wakati
Belshaza alipokuwa akinywa mvinyo
wake, aliamuru viletwe vile vikombe vya
dhahabu na fedha ambavyo Nebukadneza
baba yake alikuwa amevichukua kutoka
hekaluni huko Yerusalemu, ili mfalme na
wakuu wake, wake zake na masuria wake
waweze kuvinywea. 3 Kwa hiyo wakavileta
vile vikombe vya dhahabu ambavyo
vilikuwa vimechukuliwa kutoka Hekalu la
Mungu huko Yerusalemu, naye mfalme na
wakuu wake, wake zake na masuria wake
wakavinywea. 4 [g]Walipokuwa wakinywa
mvinyo, wakaisifu miungu ya dhahabu na
fedha, ya shaba, chuma, miti na mawe.
5 Ghafula vidole vya mkono wa
mwanadamu vilitokea na kuandika juu ya
ukuta, karibu na kinara cha taa ndani ya
jumba la mfalme. Mfalme akatazama kitanga
kilivyokuwa kikiandika. 6 [h]Uso wa mfalme
ukageuka rangi, naye akaogopa sana, kiasi
kwamba magoti yake yaligongana na miguu
yake ikalegea.
7 [i]Mfalme akawaita wasihiri, wanajimu
na waganga waletwe, naye akawaambia
hawa wenye hekima wa Babeli, "Yeyote
asomaye maandishi haya na kuniambia
maana yake atavikwa nguo za zambarau,
na kuvikwa mkufu wa dhahabu shingoni
mwake, naye atafanywa mtawala wa cheo
cha tatu katika ufalme."
8 [j]Ndipo watu wote wa mfalme wenye
hekima wakaingia, lakini hawakuweza
kusoma yale maandishi wala kumwambia
mfalme maana yake. 9 [k]Basi Mfalme
Belshaza akazidi kujawa na hofu, na uso
wake ukageuka rangi zaidi. Wakuu wake
wakapigwa na bumbuazi.

---

[a]**4:34** Dan 12:7; Ufu 4:10; Lk 1:33; Ay 12:20; Isa 37:16; Dan 6:26; Za 145:13; Dan 2:44; 5:21
[b]**4:35** Isa 40:17; Kum 21:8; Yon 1:14; Ay 9:4; Rum 9:20; Isa 14:24; 45:9; Za 115:3; 136:6; Kum 32:39; Dan 5:21
[c]**4:36** Mit 22:4; Dan 5:18; Ay 42:12
[d]**4:37** Kum 32:4; Za 33:4-5; Kut 18:11; Mt 23:12; Kut 15:2; Za 18:27; 34:3; Ay 31:4; 40:11-12; Isa 13:11; Dan 5:23; Za 119:21
[e]**5:1** 1Fal 3:15; Mk 6:21; Es 3:1; Yer 50:35; Dan 7:1; 8:1
[f]**5:2** 2Nya 36:10; Yer 52:19; Es 1:7; Mit 20:1; Isa 21:5; 2Fal 24:13; Es 2:14; Dan 1:2
[g]**5:4** Es 1:10; Ufu 9:20; Za 115:4-8; Amu 16:24; Hag 2:19; Za 135:15-18
[h]**5:6** Dan 4:5; Za 22:14; Nah 2:10; Ay 4:15; Isa 7:2; Eze 7:17
[i]**5:7** Isa 44:25; 47:13; Dan 4:6-7; Mwa 41:42; Dan 2:5-6, 48; 6:2-3; Mwa 41:8; Isa 19:3; 44:25; Yer 50:35; Es 10:3
[j]**5:8** Dan 2:10, 27; 4:18; Mwa 41:8; 41:8; Kut 8:18
[k]**5:9** Za 48:5; Isa 21:4

10 [a]Malkia[b] aliposikia sauti za mfalme
na wakuu wake, alikuja katika ukumbi
wa karamu. Akasema, “Ee mfalme, uishi
milele! Usishtuke! Usibadilike rangi kiasi
hicho! 11 [c]Yuko mtu katika ufalme wako
ambaye ana roho ya miungu mitakatifu
ndani yake. Wakati wa baba yako, mtu
huyo alionekana kuwa na ufahamu, akili
na hekima kama ile ya miungu. Mfalme
Nebukadneza baba yako, yaani nasema
mfalme baba yako, alimweka kuwa mkuu
wa waganga, wasihiri, wanajimu na
waaguzi. 12 [d]Mtu huyu Danieli, ambaye
mfalme alimwita Belteshaza, alionekana
kuwa na akili nyepesi, maarifa na ufahamu,
pia uwezo wa kufasiri ndoto, kueleza
mafumbo na kutatua matatizo magumu.
Mwite Danieli, naye atakuambia maana ya
haya maandishi.”

13 [e]Hivyo Danieli akaletwa mbele ya
mfalme, naye mfalme akamuuliza, “Je,
wewe ndiwe Danieli, mmoja wa watu wa
uhamisho walioletwa na mfalme baba yangu
kutoka Yuda? 14 Nimesikia kwamba roho ya
miungu iko ndani yako, na kwamba una
ufahamu, akili na hekima ya pekee. 15 [f]Watu
wenye hekima na wasihiri waliletwa mbele
yangu ili kusoma maandishi haya na
kuniambia maana yake, lakini hawakuweza
kunifafanulia. 16 [g]Basi nimesikia kwamba
unaweza kutoa tafsiri na kutatua matatizo
magumu. Ikiwa unaweza kusoma maandishi
haya na kuniambia maana yake, utavikwa
nguo za zambarau na mkufu wa dhahabu
shingoni mwako, nawe utafanywa mtawala
wa tatu katika ufalme.”

17 [h]Ndipo Danieli akamjibu mfalme,
“Waweza kubaki na zawadi zako mwenyewe
na kumpa mtu mwingine zawadi zako. Hata
hivyo, nitasoma maandishi kwa mfalme na
kumwambia maana yake.

18 [i]“Ee mfalme, Mungu Aliye Juu Sana
alimpa baba yako Nebukadneza utawala,
ukuu, utukufu na fahari. 19 [j]Kwa sababu ya
nafasi ya juu aliyompa baba yako, kabila
zote za watu, mataifa na watu wa kila
lugha walimhofu na kumwogopa. Wale
ambao mfalme alitaka kuwaua, aliwaua;
wale aliotaka kuwaacha hai, aliwaacha
hai; wale aliotaka kuwapandisha cheo,
aliwapandisha; aliotaka kuwashusha,
aliwashusha. 20 [k]Lakini moyo wake
ulipokuwa na majivuno na kuwa mgumu
kwa kiburi, aliondolewa kutoka kwa
kiti chake cha ufalme na kuvuliwa
utukufu wake. 21 [l]Akafukuzwa mbali na
wanadamu na kupewa akili ya mnyama,
akaishi pamoja na punda-mwitu, akala
majani kama ng’ombe, nao mwili wake
ukaloweshwa kwa umande wa mbingu,
mpaka alipotambua kwamba Mungu Aliye
Juu Sana ndiye mtawala juu ya falme za
wanadamu na kwamba humtawaza juu yao
yeyote amtakaye.

22 [m]“Lakini wewe mwanawe, ee Belshaza,
hukujinyenyekeza, ingawa ulifahamu haya
yote. 23 [n]Badala yake, umejiinua dhidi ya
Bwana wa mbingu. Uliletewa vikombe
vya Hekalu lake, nawe na wakuu wako,
wake zako na masuria wako mlivitumia
kwa kunywea mvinyo. Ukaisifu miungu
ya fedha na dhahabu, ya shaba, chuma,
miti na mawe, miungu ambayo haiwezi
kuona, au kusikia wala kufahamu.
Lakini hukumheshimu Mungu ambaye
anaushikilia uhai wako na njia zako zote
mkononi mwake. 24 Kwa hiyo ameutuma
mkono ule ulioandika maneno.

[a]**5:10** Neh 2:3; Dan 3:9
[b]10 Au: Mama yake mfalme.
[c]**5:11** Mwa 41:38; Dan 4:8-9; 1:17; 2:47-48; 2:22; Mwa 41:38; Dan 2:22
[d]**5:12** Dan 1:7; 6:3; Hes 12:8; Eze 28:3
[e]**5:13** Es 2:5-6; Dan 6:13
[f]**5:15** Dan 4:18
[g]**5:16** Mwa 41:15; 42; Es 5:3; Dan 2:6; Mwa 41:15, 42
[h]**5:17** 2Fal 5:16
[i]**5:18** Yer 27:7; Dan 4:36; Yer 28:14; Dan 2:37-38
[j]**5:19** Dan 2:12-13; 3:6; Yer 25:9; Dan 4:22
[k]**5:20** Dan 4:30; Yer 13:18; Ay 40:12; Eze 31:10-11; Isa 14:12; Yer 43:10; Dan 8:8
[l]**5:21** Eze 17:24; Kut 9:14-16; Dan 4:16-17
[m]**5:22** Kut 10:3; 2Nya 33:23
[n]**5:23** Ufu 13:6; Isa 14:13; Hes 2:19; Yer 50:29; Ufu 9:20; Ay 12:10; Mdo 17:28; Yer 44:9; Ay 31:4; Za 115:4-8; Hab 2:19; Isa 13:11; Yer 10:23; 48:26

25 “Haya ndiyo maneno yaliyoandikwa:

MENE, MENE, TEKELI NA PERESI

26 [a]“Hii ndiyo maana ya maneno haya:

“*Mene*: Mungu amezihesabu siku za
utawala wako na kuukomesha.
27 [b]*Tekeli*: Wewe umepimwa katika
mizani na umeonekana
umepungua.
28 [c]*Peresi*: Ufalme wako umegawanywa
na kupewa Wamedi na Waajemi.”

29 [d]Ndipo kwa amri ya Belshaza, Danieli
akavikwa nguo za zambarau na mkufu wa
dhahabu shingoni, tena akatangazwa kuwa
mtawala wa tatu katika ufalme.
30 [e]Usiku ule ule, Belshaza mfalme wa
Wakaldayo akauawa, 31 [f]naye Dario Mmedi
akashika ufalme akiwa na miaka sitini na
miwili.

*Danieli Katika Tundu La Simba*

6 [g]Ilimpendeza Dario kuteua wakuu 120
kutawala katika ufalme wake wote,
2 [h]pamoja na wasimamizi watatu juu yao,
ambao mmoja wao alikuwa Danieli. Wakuu
walitoa hesabu kwa hao wasimamizi ili
mfalme asipate hasara. 3 [i]Basi Danieli
alijidhihirisha, miongoni mwa wasimamizi
na wakuu kwa sifa zake za kipekee hata
mfalme akapanga kumweka juu ya ufalme
wote. 4 [j]Walipofahamu hilo, wakuu na
wasimamizi wakajaribu kutafuta sababu za
kumshtaki Danieli kuhusu usimamizi wake
wa shughuli za serikali, lakini hawakuweza
kufanikiwa. Hawakuweza kupata kosa
kwake, kwa sababu alikuwa mwaminifu,
wala hakupatikana na upotovu au uzembe.
5 [k]Mwishoni watu hawa walisema, “Kamwe
hatutapata msingi wa mashtaka dhidi ya
huyu Danieli isipokuwa iwe inahusiana na
sheria ya Mungu wake.”
6 [l]Basi wasimamizi na wakuu wakaingia
kwa mfalme kama kikundi wakasema, “Ee
Mfalme Dario, uishi milele! 7 [m]Wasimamizi
wa ufalme, wasaidizi, wakuu, washauri na
watawala wote wamekubaliana kwamba
mfalme atoe sheria na kukazia amri kuwa
yeyote atakayetoa dua kwa mungu au
mwanadamu yeyote katika muda huu wa
siku thelathini zijazo, isipokuwa kwako
wewe, ee mfalme, atupwe ndani ya tundu
la simba. 8 [n]Sasa, ee mfalme, toa amri na
uiandike ili isiweze kubadilishwa: kulingana
na sheria za Wamedi na Waajemi, ambazo
haziwezi kubatilishwa.” 9 [o]Hivyo Mfalme
Dario akaiweka amri hiyo katika maandishi.
10 [p]Basi Danieli alipofahamu kuwa amri
ile imetangazwa, alikwenda nyumbani
kwenye chumba chake cha ghorofani
ambako madirisha yalifunguka kuelekea
Yerusalemu. Akapiga magoti na kuomba
mara tatu kwa siku, akimshukuru Mungu
wake kama alivyokuwa akifanya mwanzoni.
11 [q]Ndipo watu hawa wakaenda kama
kikundi na kumkuta Danieli akiomba na
kumsihi Mungu kwa ajili ya msaada. 12 [r]Basi
wakaenda kwa mfalme na kusema naye
kuhusu amri ya mfalme: “Je, hukutangaza
amri kwamba kwa muda huu wa siku
thelathini zijazo mtu yeyote ambaye
atamwomba mungu au mwanadamu yeyote
isipokuwa wewe, ee mfalme, angetupwa
ndani ya tundu la simba?”

Mfalme akajibu, “Amri ndivyo ilivyo,
kulingana na sheria za Wamedi na Waajemi,
ambazo haziwezi kubatilishwa.”
13 [s]Ndipo wakamwambia mfalme,
“Danieli, ambaye ni mmoja wa mahamisho

[a]**5:26** Yer 27:7; Isa 13:9
[b]**5:27** Za 62:9; Yer 6:30; Ay 6:2
[c]**5:28** Isa 13:17; Yer 50:41-43; Dan 6:28; Yer 7:27
[d]**5:29** Mwa 41:42; Dan 2:6
[e]**5:30** Isa 21:9; Yer 51:31; 50:35
[f]**5:31** Yer 50:41; Dan 11:1; Isa 13:3
[g]**6:1** Dan 5:31; Es 1:1
[h]**6:2** Dan 2:48-49; Mit 3:35; Dan 5:12-14; 1:20
[i]**6:3** Es 10:3; Mwa 41:41; Mit 3:35; Dan 5:12-14; 1:20
[j]**6:4** Yer 20:10
[k]**6:5** Mdo 24:13-16
[l]**6:6** Neh 2:3; Dan 2:4
[m]**6:7** Dan 3:2; Za 59:3; 64:2-6; Dan 3:6
[n]**6:8** Es 1:19
[o]**6:9** Dan 9:23; Eze 2:1; Dan 9:23
[p]**6:10** 1Fal 8:29; Mdo 5:29; Za 95:6; Mt 6:6
[q]**6:11** 1Fal 8:48-50; Za 55:17; 1The 5:17-18
[r]**6:12** Es 1:19; Dan 3:8-12
[s]**6:13** Eze 14:14; Dan 2:25; Es 3:8; Dan 3:12

kutoka Yuda, hakuheshimu, ee mfalme, wala
hajali amri uliyoiweka kwa maandishi. Bado
anaomba mara tatu kwa siku.” 14 [a]Wakati
mfalme aliposikia hili, akahuzunika mno.
Akakusudia kumwokoa Danieli, hivyo
akafanya kila jitihada ya kumwokoa hadi
jua likatua.

15 [b]Ndipo wale watu wakamwendea
mfalme kama kikundi na kumwambia,
“Ee mfalme, kumbuka kwamba kulingana
na sheria ya Wamedi na Waajemi, hakuna
amri wala sheria ambayo mfalme ameitoa
inayoweza kubadilishwa.”

16 [c]Basi mfalme akatoa amri, nao
wakamleta Danieli, na wakamtupa ndani
ya tundu la simba. Mfalme akamwambia
Danieli, “Mungu wako unayemtumikia
daima na akuokoe!”

17 [de]Jiwe likaletwa na kuwekwa kwenye
mdomo wa tundu, naye mfalme akalitia
muhuri kwa pete yake mwenyewe pamoja
na kwa pete za wakuu wake, ili hali ya
Danieli isiweze kubadilishwa. 18 [f]Kisha
mfalme akarudi kwenye jumba lake la
kifalme, naye usiku kucha hakula chakula
wala kutumia viburudisho alivyoletewa.
Lakini hakuweza kulala.

19 Asubuhi na mapema, mfalme
akaondoka na kuharakisha kwenda kwenye
tundu la simba. 20 [g]Wakati alipokaribia lile
tundu, akamwita Danieli kwa sauti ya
uchungu, “Danieli, mtumishi wa Mungu
aliye hai! Je, Mungu wako unayemtumikia
daima, ameweza kukuokoa kwa simba?”

21 [h]Danieli akajibu, “Ee mfalme, uishi
milele! 22 [i]Mungu wangu alimtuma
malaika wake, naye akafunga vinywa vya
hawa simba. Hawajanidhuru, kwa sababu
nilionekana sina hatia mbele zake. Wala
kamwe sijafanya jambo lolote baya mbele
yako, ee mfalme.”

23 [j]Mfalme akafurahi mno, naye akatoa
amri Danieli atolewe kutoka kwa lile tundu.
Danieli alipotolewa kutoka kwa lile tundu,
hakukutwa na jeraha lolote, kwa sababu
alikuwa amemtumaini Mungu wake.

24 [k]Kwa amri ya mfalme, wale watu
waliokuwa wamemshtaki Danieli kwa
uongo waliletwa na kutupwa ndani ya
lile tundu la simba, pamoja na wake zao
na watoto wao. Nao kabla hawajafika
chini kwenye sakafu ya lile tundu, simba
wakawakamata na kusaga mifupa yao yote.

25 [l]Kisha Mfalme Dario akawaandikia
kabila zote za watu, mataifa, na watu wa
kila lugha katika nchi yote:

“Ninyi na mstawi sana!

26 [m]“Natoa amri hii, kwamba katika
kila sehemu ya ufalme wangu, lazima
watu wamwogope na kumheshimu
Mungu wa Danieli.

“Kwa maana yeye ni Mungu aliye
hai,
naye hudumu milele,
ufalme wake hautaangamizwa,
nao utawala wake hauna mwisho.
27 Huponya na kuokoa;
hufanya ishara na maajabu
mbinguni na duniani.
Amemwokoa Danieli
kutoka nguvu za simba.”

28 [n]Hivyo Danieli akastawi wakati wa
utawala wa Dario, na utawala wa Koreshi
Mwajemi.

*Ndoto Ya Danieli Ya Wanyama Wanne*

7 [o]Katika mwaka wa kwanza wa utawala
wa Belshaza mfalme wa Babeli, Danieli

[a]**6:14** Dan 3:13; Mk 6:26
[b]**6:15** Es 8:8
[c]**6:16** Ay 5:19; 2Kor 1:10; Za 97:10; 37:39-40
[d]**6:17** Mt 27:66; Mao 3:53
[e]**6:17** Dan 4:3; 3:29
[f]**6:18** 2Sam 12:17; Dan 3:10; Es 6:1; Dan 2:1
[g]**6:20** Dan 3:17; Yer 32:17; Mwa 18:14
[h]**6:21** Neh 2:3; Dan 2:4; 3:9
[i]**6:22** Dan 3:23-28; Mwa 32:1; Za 91:11-13; Ebr 11:33; Mdo 12:11; 2Tim 4:17
[j]**6:23** Dan 3:27; Mk 16:18; Isa 12:2; 1Nya 5:20
[k]**6:24** Kum 19:18-19; Es 7:9-10; 2Fal 14:6; Isa 38:13; Kum 24:16; 2Fal 14:6
[l]**6:25** Dan 3:4; 4:1
[m]**6:26** Dan 4:34; Es 8:17; Dan 2:44; Za 99:1-3; Yos 2:11; 3:10; Dan 12:7; Za 5:7; Dan 3:26; Yer 10:10; Ufu 1:18
[n]**6:28** 2Nya 36:22; Dan 1:21; 5:1, 28
[o]**7:1** Yer 36:4; Dan 1:17; Eze 40:2; Za 4:4; Dan 4:13

aliota ndoto, nayo maono yakapita
mawazoni yake alipokuwa amelala
kitandani mwake. Akayaandika mambo
aliyoyaona katika ndoto yake.
2 [a]Danieli akasema: “Katika maono yangu
usiku nilitazama, na hapo mbele yangu
kulikuwepo na upepo kutoka pande nne za
mbingu, ukivuruga bahari kuu. 3 [b]Wanyama
wanne wakubwa, kila mmoja tofauti na
mwenzake, wakajitokeza kutoka bahari.
4 [c]“Mnyama wa kwanza alifanana na
simba, naye alikuwa na mabawa kama
ya tai. Nikatazama mpaka mabawa yake
yalipong’olewa, naye akainuliwa katika
nchi, akasimama kwa miguu miwili kama
mwanadamu, naye akapewa moyo wa
binadamu.
5 [d]“Hapo mbele yangu kulikuwa na
mnyama wa pili, ambaye alionekana
kama dubu. Upande wake mmoja ulikuwa
umeinuka, na alikuwa na mbavu tatu
katika kinywa chake kati ya meno yake.
Akaambiwa, ‘Amka, ule nyama mpaka
ushibe!’
6 [e]“Baada ya huyo, nilitazama, na mbele
yangu kulikuwa na mnyama mwingine,
aliyefanana na chui. Juu ya mgongo wake
alikuwa na mabawa manne kama ya ndege.
Mnyama huyu alikuwa na vichwa vinne,
naye akapewa mamlaka ya kutawala.
7 “Baada ya huyo, katika maono yangu
usiku nilitazama, na mbele yangu kulikuwa
na mnyama wa nne, mwenye kutisha na
kuogofya, tena mwenye nguvu nyingi.
Alikuwa na meno makubwa ya chuma;
akapondaponda na kuangamiza wahanga
wake, na kukanyaga chini ya nyayo zake
chochote kilichosalia. Alikuwa tofauti na
wanyama wote waliotangulia, naye alikuwa
na pembe kumi.
8 [f]“Wakati nilipokuwa ninafikiri kuhusu
pembe hizo, mbele yangu kulikuwa
na pembe nyingine, ambayo ni ndogo,
iliyojitokeza miongoni mwa zile kumi;
pembe tatu za mwanzoni ziling’olewa ili
kuipa nafasi hiyo ndogo. Pembe hii ilikuwa
na macho kama ya mwanadamu, na mdomo
ulionena kwa majivuno.
9 [g]“Nilipoendelea kutazama,

“viti vya enzi vikawekwa,
naye Mzee wa Siku akaketi.
Mavazi yake yalikuwa meupe kama
theluji;
nywele za kichwa chake zilikuwa
nyeupe kama sufu.
Kiti chake cha enzi kilikuwa
kinawaka kwa miali ya moto,
nayo magurudumu yake yote
yalikuwa yanawaka moto.
10 [h]Mto wa moto ulikuwa unatiririka,
ukipita mbele yake.
Maelfu elfu wakamhudumia;
kumi elfu mara kumi elfu
wakasimama mbele zake.
Mahakama ikakaa kuhukumu,
na vitabu vikafunguliwa.

11 [i]“Kisha nikaendelea kutazama kwa
sababu ya yale maneno ya majivuno
yaliyosemwa na ile pembe. Nikaendelea
kuangalia mpaka yule mnyama alipouawa,
na mwili wake ukaharibiwa na kutupwa
katika ule moto uliowaka. 12 (Wanyama
wengine walikuwa wamevuliwa mamlaka
yao, lakini waliruhusiwa kuishi kwa muda
fulani.)
13 [j]“Katika maono yangu ya usiku
nilitazama, na mbele yangu nikamwona
anayefanana na mwanadamu, akija pamoja
na mawingu ya mbinguni. Akamkaribia
huyo Mzee wa Siku, na akaongozwa mbele
zake. 14 [k]Akapewa mamlaka, utukufu na
ufalme wenye nguvu; nao watu wa kabila
zote, mataifa, na watu wa kila lugha

[a]**7:2** Eze 37:9; Dan 11:4; 8:8; Ufu 7:1
[b]**7:3** Ufu 13:1; Zek 6:1-4
[c]**7:4** Zek 7:2; Eze 17:3; Ufu 13:2; Yer 4:2; 2Fal 24:1; Yer 4:7
[d]**7:5** Dan 2:39
[e]**7:6** Ufu 13:2
[f]**7:8** Dan 8:9; Ufu 9:7; Za 12:3; Ufu 13:5-6
[g]**7:9** Ufu 1:14; Eze 1:15; 10:6; 1Fal 22:19; 2Nya 18:18; Mt 19:28
[h]**7:10** Za 50:3; Isa 30:27; Kum 33:2; Yud 14; Ufu 5:11; Kut 32:32; Ufu 20:11-15
[i]**7:11** Ufu 19:20; 13:5-6
[j]**7:13** Eze 1:26; Mt 8:20; 24:30; Kum 33:26; Ufu 1:13; 14:14; Isa 13:6
[k]**7:14** Yn 3:35; Ebr 12:28; Dan 2:44; Mt 28:18; Efe 1:22; Za 72:11; Isa 16:5

wakamwabudu. Utawala wake ni utawala
wa milele ambao hautapita, nao ufalme
wake ni ule ambao kamwe hautaangamizwa.

*Tafsiri Ya Ndoto*

15 [a]“Mimi, Danieli, nilipata mahangaiko
rohoni, nayo maono yale yaliyopita
ndani ya mawazo yangu yalinisumbua.
16 [b]Nikamkaribia mmoja wa wale
waliosimama pale na kumuuliza maana
halisi ya haya yote.

“Basi akaniambia na kunipa tafsiri ya vitu
hivi: 17 ‘Hao wanyama wanne wakubwa ni
falme nne zitakazoinuka duniani. 18 [c]Lakini
watakatifu wa Yeye Aliye Juu Sana
watapokea ufalme na kuumiliki milele:
naam, milele na milele.’

19 “Kisha nilitaka kufahamu maana ya
kweli ya mnyama yule wa nne, ambaye
alikuwa tofauti na wale wengine wote, tena
wa kutisha sana, na meno yake ya chuma
na makucha ya shaba: mnyama ambaye
alipondaponda na kuangamiza wahanga
wake, na kukanyaga chochote kilichosalia.
20 [d]Pia mimi nilitaka kujua kuhusu zile
pembe kumi juu ya kichwa chake, na pia
kuhusu ile pembe nyingine iliyojitokeza,
ambayo mbele yake zile tatu za mwanzoni
zilianguka, ile pembe ambayo ilionekana
kuvutia macho zaidi kuliko zile nyingine,
na ambayo ilikuwa na macho na kinywa
kilichonena kwa majivuno. 21 [e]Nilipoendelea
kutazama, pembe hii ilikuwa inapigana
vita dhidi ya watakatifu na kuwashinda,
22 [f]mpaka huyo Mzee wa Siku alipokuja
na kutamka hukumu kwa kuwapa ushindi
watakatifu wa Yeye Aliye Juu Sana, na
wakati ukawadia walipoumiliki ufalme.

23 [g]“Alinipa maelezo haya: ‘Mnyama wa
nne ni ufalme wa nne ambao utatokea
duniani. Utakuwa tofauti na falme
nyingine zote, nao utaharibu dunia nzima,
ukiikanyaga chini na kuipondaponda.
24 [h]Zile pembe kumi ni wafalme kumi
watakaotokana na ufalme huu. Baada
yao mfalme mwingine atainuka, ambaye
atakuwa tofauti na wale waliotangulia,
naye atawaangusha wafalme watatu.
25 [i]Atanena maneno kinyume cha Yeye Aliye
Juu Sana na kuwaonea watakatifu wake,
huku akijaribu kubadili majira na sheria.
Watakatifu watatiwa chini ya mamlaka
yake kwa wakati, nyakati mbili, na nusu
wakati.[j]

26 [k]“ ‘Lakini mahakama itakaa kuhukumu,
nayo mamlaka yake yataondolewa na
kuangamizwa kabisa milele. 27 [l]Ndipo
ufalme, mamlaka na ukuu wa falme chini ya
mbingu yote utakabidhiwa kwa watakatifu,
watu wa Yeye Aliye Juu Sana. Ufalme wake
utakuwa ufalme wa milele, nao watawala
wote watamwabudu na kumtii yeye.’

28 [m]“Huu ndio mwisho wa jambo lile. Mimi
Danieli nilitaabika sana katika mawazo
yangu, nao uso wangu ukabadilika, lakini
nililiweka jambo hilo moyoni mwangu.”

*Maono Ya Danieli Ya Kondoo Dume Na Beberu*

8 [n]Katika mwaka wa tatu wa utawala
wa Mfalme Belshaza, mimi Danieli,
nilipata maono, baada ya maono ambayo
yalikuwa yamenitokea mbeleni. 2 [o]Katika
maono yangu, nilijiona nikiwa ndani
ya ngome ya Shushani katika jimbo la
Elamu. Katika maono nilikuwa kando ya
Mto Ulai.[p] 3 [q]Nikatazama juu, na hapo

---

[a]**7:15** Ay 4:15; Dan 4:19
[b]**7:16** Dan 9:22; Zek 1:9; Dan 8:16
[c]**7:18** Isa 60:12-14; Lk 12:32; Za 16; 3; 49:14; Ebr 12:28
[d]**7:20** Ufu 17:12; 13:5-6
[e]**7:21** Ufu 13:7; 11:7
[f]**7:22** Mk 8:35
[g]**7:23** Dan 2:40
[h]**7:24** Ufu 17:12
[i]**7:25** Isa 37:23; Dan 11:36; 2:21; 12:7-13; Ufu 16:6; Lk 21:8; Mdo 1:6-7; Ufu 11:2
[j]25 Wakati, nyakati mbili, na nusu wakati maana yake ni mwaka mmoja, miaka miwili, na nusu mwaka, yaani miaka mitatu na nusu.
[k]**7:26** Ufu 19:20
[l]**7:27** 2Sam 7:13; Lk 1:33; Za 22:27; 72:11; Isa 14:2; 1Kor 6:2; Mwa 14:18
[m]**7:28** Isa 21:3; Dan 4:19; Lk 2:19; Za 13:2; Ay 4:15
[n]**8:1** Dan 5:1
[o]**8:2** Mwa 10:22; Es 2:8; Ezr 4:9
[p]2 Mto Ulai ni mfereji uliokuwa kati ya Shushani na Elymaisi; sasa unaitwa Mto Karuni.
[q]**8:3** Dan 10:5; Ufu 13:11

mbele yangu kulikuwa na kondoo dume
mwenye pembe mbili, akiwa amesimama
kando ya mto, nazo pembe zake zilikuwa
ndefu. Pembe moja ilikuwa ndefu kuliko
hiyo nyingine, lakini iliendelea kukua
baadaye. 4 [a]Nikamtazama yule kondoo
dume alivyokuwa akishambulia kuelekea
magharibi, kaskazini na kusini. Hakuna
mnyama yeyote aliyeweza kusimama dhidi
yake, wala hakuna aliyeweza kuokoa kutoka
nguvu zake. Alifanya kama atakavyo, naye
akawa mkuu.
5 Nilipokuwa ninatafakari hili, ghafula
beberu mwenye pembe moja kubwa sana
katikati ya macho yake alikuja kutoka
magharibi, akiruka kasi juu ya dunia yote
bila kugusa ardhi. 6 Alikuja akimwelekea
yule kondoo dume mwenye pembe
mbili niliyemwona akisimama kando ya
mto, akamshambulia kwa hasira nyingi.
7 [b]Nikamwona akimshambulia yule kondoo
dume kwa hasira nyingi, akimpiga yule
kondoo dume na kuvunja pembe zake mbili.
Yule kondoo dume hakuwa na nguvu za
kumzuia yule beberu, hivyo akamwangusha
yule kondoo dume chini na kumkanyaga,
wala hakuna aliyeweza kumwokoa yule
kondoo dume kutoka nguvu za huyo
beberu. 8 [c]Yule beberu akawa mkubwa
sana, lakini katika kilele cha nguvu zake
ile pembe yake ndefu ilivunjika, na mahali
pake pakaota pembe nne kubwa kuelekea
pande nne za dunia.
9 [d]Kutoka mojawapo ya zile pembe nne
palitokea pembe ndogo ukaongezeka nguvu
kuelekea kusini, na kuelekea mashariki, na
kuelekea Nchi ya Kupendeza. 10 [e]Pembe
hiyo ikaendelea kukua hadi kufikia
jeshi la mbinguni, nayo ikalitupa baadhi
ya jeshi la vitu vya angani hapa chini
duniani, na kulikanyaga. 11 [f]Pembe hiyo
ikajikweza ili iwe kama Mkuu wa hilo jeshi;
ikamwondolea dhabihu ya kila siku, napo
mahali pake patakatifu pakashushwa chini.
12 Kwa sababu ya uasi, jeshi la watakatifu
na dhabihu za kila siku vikatiwa mikononi
mwake. Ikafanikiwa katika kila kitu
ilichofanya, nayo kweli ikatupwa chini.
13 [g]Kisha nikamsikia mtakatifu mmoja
akizungumza na mtakatifu mwingine,
akamwambia, "Je, itachukua muda gani
maono haya yatimie: maono kuhusu
dhabihu ya kila siku, uasi unaosababisha
ukiwa, kutwaliwa kwa mahali patakatifu,
na jeshi litakalokanyagwa chini ya nyayo?"
14 [h]Akaniambia, "Itachukua siku 2,300.
Ndipo mahali patakatifu patawekwa wakfu
tena."

*Tafsiri Ya Maono*

15 [i]Mimi Danieli nilipokuwa ninaangalia
maono na kujaribu kuelewa, mbele
yangu alisimama mmoja aliyefanana na
mwanadamu. 16 [j]Kisha nikasikia sauti
ya mwanadamu kutoka Mto Ulai ikiita,
"Gabrieli, mwambie mtu huyu maana ya
maono haya."
17 [k]Alipokuwa akikaribia pale nilipokuwa
nimesimama, niliogopa, nikaanguka
kifudifudi. Akaniambia, "Mwana wa
mwanadamu, fahamu kuwa maono haya
yanahusu siku za mwisho."
18 [l]Alipokuwa akinena nami, nilikuwa
katika usingizi mzito, huku nimelala
kifudifudi. Ndipo aliponigusa na
kunisimamisha wima.
19 [m]Akaniambia, "Nitakuambia yale
yatakayotokea baadaye wakati wa
ghadhabu, kwa sababu maono haya
yanahusu wakati wa mwisho ulioamriwa.
20 [n]Kondoo dume mwenye pembe mbili
ambaye ulimwona anawakilisha wafalme

[a]**8:4** Dan 11:3, 16; Isa 41:3
[b]**8:7** Dan 7:7; 11:11
[c]**8:8** 2Nya 26:16-21; Dan 5:20; 7:2; Ufu 7:1
[d]**8:9** Eze 20:6; Dan 11:16; Za 48:2; Dan 7:8
[e]**8:10** Isa 14:13; Ufu 8:10; 12:4; Dan 7:7
[f]**8:11** Dan 11:36-37; Eze 46:13-14; Dan 12:11; 11:31
[g]**8:13** Kum 33:2; Dan 4:23; 12:6; Lk 21:24; Isa 28:18; Ufu 11:2
[h]**8:14** Dan 12:11-12
[i]**8:15** Eze 2:1; Dan 10:16-18
[j]**8:16** Dan 9:21; Lk 1:19; Dan 7:16
[k]**8:17** Eze 44:4; Ufu 1:17; Hab 2:3; Eze 1:28; Dan 2:46
[l]**8:18** Dan 10:9; Eze 2:2; Zek 4:1
[m]**8:19** Isa 10:25; Za 102:13
[n]**8:20** Eze 27:10

wa Umedi na Uajemi. 21 [a]Yule beberu
mwenye nywele nyingi ni mfalme wa
Uyunani, nayo ile pembe ndefu katikati
ya macho yake ni mfalme wa kwanza.
22 Zile pembe nne zilizoota badala ya ile
pembe iliyovunjika zinawakilisha falme nne
ambazo zitatokea kutoka taifa lake, lakini
hakuna hata mmoja utakaokuwa na nguvu
kama ule uliovunjika.
23 “Katika sehemu ya mwisho ya utawala
wao, wakati waasi watakapokuwa waovu
kabisa, atainuka mfalme mwenye uso
mkali, aliye stadi wa hila. 24 [b]Atakuwa na
nguvu nyingi, lakini si kwa uwezo wake
mwenyewe. Atasababisha uharibifu wa
kutisha, na atafanikiwa kwa chochote
anachofanya. Atawaangamiza watu maarufu
na watu watakatifu. 25 [c]Atasababisha
udanganyifu ustawi, naye atajihesabu
mwenyewe kuwa bora. Wakati wajisikiapo
kuwa wako salama, atawaangamiza wengi,
na kushindana na Mkuu wa wakuu. Lakini
ataangamizwa, isipokuwa si kwa uwezo wa
mwanadamu.
26 [d]“Maono kuhusu jioni na asubuhi
ambayo umepewa ni kweli, lakini yatie
muhuri maono haya, kwa maana yanahusu
wakati mrefu ujao.”
27 [e]Mimi Danieli nilikuwa nimechoka
sana, na nikalala nikiwa mgonjwa kwa siku
kadhaa. Ndipo nikaamka, nikaenda kwenye
shughuli za mfalme. Nilifadhaishwa na
maono hayo, nami sikuweza kuyaelewa.

*Maombi Ya Danieli*

9 [f]Katika mwaka wa kwanza wa utawala
wa Dario mwana wa Ahasuero (mzaliwa
wa Umedi), ambaye alifanywa mtawala juu
ya ufalme wa Babeli, 2 [g]katika mwaka wa
kwanza wa utawala wake, mimi Danieli
nilielewa kutokana na Maandiko, kulingana
na neno la BWANA alilopewa nabii Yeremia,
kwamba ukiwa wa Yerusalemu ungetimizwa
kwa miaka sabini. 3 [h]Kwa hiyo nikamgeukia
BWANA Mungu na kumsihi katika maombi
na dua, katika kufunga, na kuvaa nguo ya
gunia na kujipaka majivu.
4 [i]Nikamwomba BWANA Mungu wangu
na kutubu:

“Ee Bwana, Mungu mkuu na
unayetisha, anayeshika agano lake la
upendo kwao wanaompenda na kutii
maagizo yake, 5 [j]tumetenda dhambi
na kufanya mabaya. Tumekuwa
waovu na tumeasi; tumegeuka mbali
na maagizo yako na sheria zako.
6 [k]Hatukuwasikiliza watumishi wako
manabii, ambao kwa jina lako walisema
na wafalme wetu, wakuu wetu, baba
zetu, na watu wote wa nchi.
7 [l]“Bwana, wewe ni mwenye haki,
lakini siku hii ya leo tumefunikwa na
aibu: tukiwa wanaume wa Yuda, na
watu wa Yerusalemu, na Israeli yote,
wote walio karibu na walio mbali,
katika nchi zote ulikotutawanya kwa
sababu ya kukosa uaminifu kwako.
8 [m]Ee BWANA, sisi na wafalme wetu,
wakuu wetu na baba zetu tumefunikwa
na aibu kwa sababu tumefanya dhambi
dhidi yako. 9 [n]BWANA Mungu wetu ni
mwenye rehema na anayesamehe,
hata ingawa tumefanya uasi dhidi
yake. 10 [o]Hatukumtii BWANA Mungu
wetu wala kuzishika sheria alizotupa
kupitia kwa watumishi wake manabii.

[a]**8:21** Dan 10:20; 11:2
[b]**8:24** Dan 7:25; 2:34; 11:21; Ay 34:7
[c]**8:25** Dan 11:36; 11:21; Ay 34:20
[d]**8:26** Isa 8:16; Ufu 10:4; Dan 10:14; Eze 12:27; Isa 29:11; Ufu 22:10
[e]**8:27** Dan 2:47-48; Isa 21:3; Dan 7:28; 10:8; 4:19
[f]**9:1** Dan 5:31; Ezr 4:6
[g]**9:2** Yer 29:10; Zek 7:5; Yer 25:11-12; 2Nya 36:21
[h]**9:3** 2Sam 13:19; Neh 1:4; 2Nya 20:3; Yer 29:12; Dan 10:12; Yon 3:6
[i]**9:4** Kum 7:9, 21; 1Fal 8:23, 30
[j]**9:5** Isa 53:6; Mao 1:20; Za 106:6; Mao 3:42; Ezr 9:6; Yer 8:14
[k]**9:6** Yer 44:5; Yak 5:10; 2Fal 18:12; Ufu 10:7; 2Nya 36:16
[l]**9:7** Ezr 9:7; Za 44:15; Kum 4:27; Amo 9:9; Eze 39:23-24; Yer 24:9; Isa 42:6
[m]**9:8** Neh 9:33; Yer 14; 20; Eze 16:63
[n]**9:9** Kut 34:7; Hes 14:18; Neh 9:17; Yer 14:7; Za 130:4; Yer 42:12; 2Sam 24:14
[o]**9:10** 2Fal 18:12; Ufu 10:7; 2Fal 17:13-15

11 [a]Israeli yote imekosea sheria yako
na kugeuka mbali, nao wamekataa
kukutii.
“Kwa hiyo laana na viapo vya hukumu
vilivyoandikwa katika Sheria ya Mose,
mtumishi wa Mungu, vimemiminwa
juu yetu, kwa sababu tumefanya
dhambi dhidi yako. 12 [b]Umetimiza
maneno uliyosema dhidi yetu na dhidi
ya watawala wetu, kwa kuleta maafa
makubwa juu yetu. Chini ya mbingu
yote kamwe hapajatendeka kitu kama
kile kilichotendeka kwa Yerusalemu.
13 [c]Kama vile ilivyoandikwa katika
sheria ya Mose, misiba hii yote imekuja
juu yetu, lakini hatujaomba fadhili kwa
Bwana Mungu wetu kwa kugeuka
kutoka dhambi zetu na kuwa wasikivu
katika kweli yake. 14 [d]Bwana hakusita
kuleta maafa juu yetu, kwa maana
Bwana Mungu wetu ni mwenye haki
katika kila afanyalo; lakini hata hivyo
hatujamtii.
15 [e]“Sasa, Ee Bwana Mungu wetu,
ambaye uliwatoa watu wako Misri
kwa mkono wenye nguvu, na ambaye
umejifanyia Jina linalodumu mpaka
leo, tumetenda dhambi, tumefanya
mabaya. 16 [f]Ee Bwana, wewe kwa
kadiri ya matendo yako ya haki, ondoa
hasira yako na ghadhabu yako juu ya
Yerusalemu, mji wako, mlima wako
mtakatifu. Dhambi zetu na maovu ya
baba zetu yameifanya Yerusalemu na
watu wako kitu cha kudharauliwa kwa
wale wote wanaotuzunguka.
17 [g]“Basi Mungu wetu, sasa sikia
maombi na dua ya mtumishi wako.
Ee Bwana, kwa ajili yako angalia
kwa huruma ukiwa wa mahali pako
patakatifu. 18 [h]Ee Mungu, tega sikio
na ukasikie; fumbua macho yako
ukaone ukiwa wa mji ule wenye Jina
lako. Hatukutolei maombi yetu kwa
sababu sisi tuna haki, bali kwa sababu
ya rehema zako nyingi. 19 [i]Ee Bwana,
sikiliza! Ee Bwana, samehe! Ee Bwana,
sikia na ukatende! Kwa ajili yako, Ee
Mungu wangu, usikawie, kwa sababu
mji wako na watu wako wanaitwa kwa
Jina lako.”

*Majuma Sabini*

20 [j]Basi, nilipokuwa bado nikinena na
kuomba, nikiungama dhambi yangu na
dhambi ya watu wangu Israeli, na nikifanya
maombi yangu kwa Bwana Mungu wangu
kwa ajili ya mlima wake mtakatifu,
21 [k]wakati nilipokuwa bado katika maombi,
Gabrieli, yule mtu niliyekuwa nimemwona
katika maono hapo awali, alinijia kwa kasi
karibu wakati wa kutoa dhabihu ya jioni.
22 [l]Akanielimisha na kuniambia, “Danieli,
sasa nimekuja kukupa akili na ufahamu.
23 [m]Mara ulipoanza kuomba, jibu lilitolewa,
ambalo nimekuja kukupasha habari, kwa
maana wewe unapendwa sana. Kwa hiyo,
tafakari ujumbe huu na uelewe maono
haya:
24 [n]“Majuma sabini yameamriwa kwa ajili
ya watu wako na kwa ajili ya mji wako
mtakatifu, ili kumaliza makosa, kukomesha
dhambi, kufanya upatanisho kwa ajili ya
uovu, kuleta haki ya milele, kutia muhuri
maono na unabii, na pia kumtia mafuta
yeye aliye mtakatifu sana.
25 [o]“Ujue na kuelewa hili: Tangu kutolewa
kwa amri ya kuutengeneza na kuujenga

[a]**9:11** Isa 1:4-7; Yer 8:5-10; Kum 27:15-26; Yer 2:29; 2Fal 22:16; Kum 11:26; 28:15; 2Fal 17:23
[b]**9:12** Isa 44:26; Yoe 2:2; Zek 1:6; 7:12; Mao 2:17; Yer 30:7; 4:23; Dan 12:1
[c]**9:13** Isa 9:13; Yer 2:30; Isa 31:1; Kum 4:29
[d]**9:14** Yer 18:8; 44:27; Neh 9:33; Yer 32:23; Mwa 18:25; 2Nya 12:6; Yer 40:3
[e]**9:15** Kut 3:20; Yer 32:21; Neh 9:10
[f]**9:16** Amu 5:11; Kut 15:17; Zek 8:2; Za 39:8; Eze 5:14; Isa 5:25
[g]**9:17** Hes 6:24-26; Za 80:19
[h]**9:18** Za 80:14; Kum 28:10; Isa 37:17; Yer 7:10-12; 25:29; Lk 18:13
[i]**9:19** Za 44:23; 1Sam 12:22
[j]**9:20** Za 145:18; Isa 58:9; Ezr 10:1
[k]**9:21** Dan 8:16; Lk 1:19; Kut 29:39
[l]**9:22** Dan 7:16; 10:14; Amu 3:7
[m]**9:23** Dan 10:19; Lk 1:24; Dan 10:11-12; Mt 24:15; Isa 65:24
[n]**9:24** Isa 53:10; 56:1; Ebr 9:12; Isa 1:26
[o]**9:25** Ezr 4:24; 6:15; Yn 4:25; 1Sam 13:14; Ezr 3:3

upya Yerusalemu mpaka kuja kwa Mpakwa
mafuta, aliye mtawala, kutakuwako majuma
saba na majuma sitini na mawili. Barabara
zitajengwa tena pamoja na mahandaki,
lakini katika wakati wa taabu. 26 [a]Baada ya
majuma sitini na mawili, Mpakwa Mafuta
atakatiliwa mbali, wala hatabaki na kitu.
Watu wa mtawala atakayekuja watauharibu
mji pamoja na mahali patakatifu. Mwisho
utakuja kama mafuriko: Vita vitaendelea
mpaka mwisho, nao ukiwa umeamriwa.
27 [b]Mtawala huyo atathibitisha agano
na watu wengi kwa juma moja. Katikati
ya juma hilo atakomesha dhabihu na
sadaka. Mahali pa dhabihu katika Hekalu
atasimamisha chukizo la uharibifu, hadi
mwisho ulioamriwa utakapomiminwa juu
yake yeye aletaye uharibifu."

*Maono Ya Danieli Kuhusu Mtu*

10 [c]Katika mwaka wa tatu wa utawala wa
Koreshi mfalme wa Uajemi, Danieli
(ambaye aliitwa Belteshaza) alipewa
ufunuo. Ujumbe wake ulikuwa kweli, nao
ulihusu vita vikubwa. Ufahamu wa ujumbe
ulimjia katika maono.

2 [d]Wakati huo, mimi Danieli nikaomboleza
kwa majuma matatu. 3 [e]Sikula chakula
kizuri; nyama wala divai havikugusa
midomo yangu; nami sikujipaka mafuta
kamwe mpaka majuma matatu yalipotimia.

4 [f]Kwenye siku ya ishirini na nne ya
mwezi wa kwanza, nilipokuwa nimesimama
kwenye ukingo wa mto mkubwa Hidekeli,[g]
5 [h]nikatazama juu, na mbele yangu
alikuwepo mtu aliyevaa mavazi ya kitani
na mshipi wa dhahabu safi kutoka ufazi
kiunoni mwake. 6 [i]Mwili wake ulikuwa
kama kito cha zabarajadi safi, uso wake
kama umeme wa radi, macho yake kama
mwali wa moto, mikono yake na miguu
yake kama mng'ao wa shaba iliyosuguliwa
sana, nayo sauti yake kama ya umati
mkubwa wa watu.

7 [j]Mimi Danieli, ni mimi peke yangu
niliyeona hayo maono; watu waliokuwa
pamoja nami hawakuyaona, lakini
waligubikwa na hofu kuu, hata wakakimbia
na kujificha. 8 [k]Kwa hiyo niliachwa peke
yangu, nikikodolea macho maono hayo
makubwa; sikubakiwa na nguvu, na rangi
ya uso wangu ikabadilika kama aliyekufa,
nikakosa nguvu. 9 [l]Kisha nikamsikia
akisema, nami nilipokuwa nikimsikiliza,
nikalala kifudifudi, nikapatwa na usingizi
mzito.

10 [m]Mkono ulinigusa, ukaninyanyua,
na kuniweka nikipiga magoti na mikono
yangu ikashika chini, huku nikiwa bado
ninatetemeka. 11 Akasema, "Danieli, wewe
mtu upendwaye sana, fikiri kwa makini
maneno ninayokwenda kunena nawe
sasa; simama wima, kwa maana sasa
nimetumwa kwako." Naye aliponiambia
haya, nikasimama nikitetemeka.

12 [n]Ndipo akaendelea kusema, "Danieli,
usiogope. Tangu siku ya kwanza ulipotia
moyo wako ili kupata ufahamu na
kujinyenyekeza mbele ya Mungu wako,
maneno yako yalisikiwa, nami nimekuja
ili kujibu maneno yako. 13 [o]Lakini mkuu
wa ufalme wa Uajemi alinipinga kwa siku
ishirini na moja. Ndipo Mikaeli, mmoja
wa malaika wakuu, alikuja kunisaidia,
kwa sababu nilikuwa nimezuiliwa huko
na mfalme wa Uajemi. 14 [p]Sasa nimekuja
kukuelezea mambo yatakayowatokea watu
wako wakati ujao, kwa maana maono hayo
yanahusu wakati ambao haujaja bado."

---

[a]**9:26** Isa 53:8; Mt 16:21; Isa 28:2; Nah 1:8; Dan 1:8; 11:10; Za 46:8; Zek 4:14; Hag 2:23
[b]**9:27** Isa 10:22
[c]**10:1** Dan 1:7, 21; 8:26
[d]**10:2** Ezr 9:4
[e]**10:3** Dan 6:18
[f]**10:4** Mwa 2:14; Dan 2:15; 12:5
[g]4 Hedekeli ndio Mto Tigrisi.
[h]**10:5** Ezr 9:2; Ufu 15:6; Yer 10:9; Dan 8:3
[i]**10:6** Mt 17:2; 28:3; Ay 41:19; 19:12; Ufu 19:12; 1:15; Kut 28:20; Eze 1:24
[j]**10:7** 2Fal 6:17-20; Mdo 9:2
[k]**10:8** Mwa 32:24; Ay 4:14; Dan 8:27; Hes 3:16; Ay 4:15; Hab 3:16
[l]**10:9** Dan 8:18; Mt 17:6; Wim 5:2
[m]**10:10** Yer 1:9; Ufu 1:17
[n]**10:12** Law 16:31; Dan 9:3, 20; Mt 14:27; Isa 65:24
[o]**10:13** Dan 12:1; Yud 9; Isa 24:21
[p]**10:14** Dan 9:22; 2:28; Hab 2:3; Dan 8:26; Eze 12:27

15 [a]Alipokuwa akinielezea haya, nilisujudu
uso wangu ukiwa umeelekea chini, nikawa
bubu. 16 [b]Ndipo mmoja aliyeonekana kama
mwanadamu akanigusa midomo yangu,
nami nikafungua kinywa changu, nikaanza
kunena. Nikamwambia yule aliyesimama
mbele yangu, “Nimepatwa na huzuni
kubwa kwa sababu ya maono haya, bwana
wangu, nami nimeishiwa nguvu. 17 [c]Bwana
wangu, mimi mtumishi wako nitawezaje
kuzungumza na wewe? Nguvu zangu
zimeniishia hata ninashindwa kupumua.”
18 [d]Tena yule aliyeonekana kama
mwanadamu akanigusa na kunitia nguvu.
19 [e]Akasema, “Ee mtu upendwaye sana,
usiogope. Amani iwe kwako! Uwe na nguvu
sasa; jipe nguvu.”

Alipozungumza nami, nilipata nguvu,
nikasema, “Nena, bwana wangu, kwa kuwa
umenipa nguvu.”

20 [f]Kwa hiyo akasema, “Je, unajua kwa
nini nimekujia? Sasa hivi nitarudi kupigana
dhidi ya mkuu wa Uajemi, nami nikienda,
mkuu wa Uyunani atakuja. 21 [g]Lakini
kwanza nitakuambia kile kilichoandikwa
katika Kitabu cha Kweli. (Hakuna hata
mmoja anayenisaidia dhidi yao isipokuwa
Mikaeli, mkuu wenu.

11 [h]Nami katika mwaka wa kwanza wa
utawala wa Dario Mmedi, nilisimama
kumsaidia na kumlinda.)

### *Wafalme Wa Kusini Na Wa Kaskazini*

2 [i]“Sasa basi, ninakuambia kweli:
Wafalme watatu zaidi watatokea Uajemi,
kisha atatokea mfalme wa nne, ambaye
atakuwa tajiri sana kuliko wengine wote.
Wakati atakapokuwa amekwisha kujipatia
nguvu kwa utajiri wake, atamchochea kila
mmoja dhidi ya ufalme wa Uyunani. 3 [j]Ndipo
mfalme mwenye nguvu atatokea, ambaye
atatawala kwa nguvu nyingi na kufanya
anavyopenda. 4 [k]Baada ya kujitokeza, milki
yake itavunjwa na kugawanyika katika
pande nne za mbinguni. Hautakwenda
kwa wazao wake, wala hautakuwa na
nguvu alizotumia, kwa sababu milki yake
itang’olewa na kupewa wengine.

5 “Mfalme wa Kusini atakuwa na nguvu,
lakini mmoja wa majemadari wake atakuwa
na nguvu zaidi kuliko mfalme, naye
atatawala ufalme wake mwenyewe kwa
nguvu nyingi. 6 Baada ya miaka kadha,
wataungana. Binti wa mfalme wa Kusini
ataolewa kwa mfalme wa Kaskazini ili
kuimarisha mapatano, lakini huyo binti
nguvu zake hazitadumu; hata mfalme
hatadumu wala nguvu zake. Katika siku hizo
atafukuzwa, pamoja na hao wasindikizaji
wake wa kifalme, watoto wake, na yeyote
aliyemuunga mkono.

7 “Mmoja kutoka jamaa ya huyo binti
atainuka na kuchukua nafasi yake.
Atashambulia majeshi ya mfalme wa
Kaskazini na kuingia katika ngome yake;
atapigana dhidi yao naye atashinda. 8 [l]Tena
ataitwaa miungu yao, vinyago vyao vya
chuma, na vitu vyao vya thamani vya
fedha na dhahabu, na kuvichukua hadi
Misri. Kwa miaka kadha atamwacha
mfalme wa Kaskazini bila kumsumbua.
9 Kisha mfalme wa Kaskazini atashambulia
nchi ya mfalme wa Kusini, lakini atarudi
nyuma hadi kwenye nchi yake. 10 [m]Wana
wa mfalme wa Kaskazini watajiandaa kwa
vita na kukusanya jeshi kubwa, ambalo
litafagia nchi kama mafuriko yasiyozuilika
na kuendelea na vita hadi kwenye ngome
ya mfalme wa Kusini.

11 [n]“Kisha mfalme wa Kusini atatoka
kwa ghadhabu na kupigana dhidi ya
mfalme wa Kaskazini, ambaye ataunda
jeshi kubwa, lakini litashindwa. 12 Wakati
jeshi litakapokuwa limechukuliwa, mfalme

---

[a]**10:15** Eze 24:27; Lk 1:20; Dan 8:18
[b]**10:16** Isa 6:7; 21:3; Yer 1:9; Dan 8:15-18
[c]**10:17** Dan 4:19
[d]**10:18** Dan 8:18
[e]**10:19** Kut 14:13; Amu 6:23; Isa 35:4; 6:1-8; Yos 1:9; Rum 8:31; Dan 9:23
[f]**10:20** Dan 8:21; 11:2
[g]**10:21** Dan 11:2; Yud 9
[h]**11:1** Dan 5:31
[i]**11:2** Dan 10:20-21
[j]**11:3** Dan 8:4, 21
[k]**11:4** Dan 7:2; 8:22; Yer 42:10
[l]**11:8** Isa 37:19; 46:1-2; Yer 43:12
[m]**11:10** Isa 8:8; Yer 46:8; Dan 9:26
[n]**11:11** Dan 8:7-8

wa Kusini atajawa na kiburi na atachinja maelfu mengi, hata hivyo hatabaki na ushindi. [13] Kwa maana mfalme wa Kaskazini atakusanya jeshi jingine kubwa kuliko lile la kwanza; na baada ya miaka kadha, atasonga mbele na jeshi kubwa mno lililoandaliwa vizuri.

[14] “Katika nyakati hizo wengi watainuka dhidi ya mfalme wa Kusini. Watu wenye ghasia miongoni mwa watu wako mwenyewe wataasi ili kutimiza maono, lakini bila mafanikio. [15] [a]Ndipo mfalme wa Kaskazini atakuja na kuuzunguka mji kwa majeshi, na kuuteka mji wa ngome. Majeshi ya Kusini yatakosa nguvu za kuyazuia; naam, hata vikosi vyao vya askari vilivyo bora zaidi, havitakuwa na nguvu ya kuwakabili. [16] [b]Huyo mvamia nchi atafanya apendavyo; hakuna yeyote atakayeweza kumpinga. Atajiimarisha katika Nchi ya Kupendeza, na atakuwa na uwezo wa kuiangamiza. [17] [c]Ataamua kuja na nguvu za ufalme wake wote na kufanya mapatano ya amani na mfalme wa Kusini. Naye atamtoa binti yake aolewe naye ili kuuangusha ufalme, lakini mipango yake haitafanikiwa wala kumsaidia. [18] [d]Ndipo atabadili nia yake kupigana na nchi za pwani na ataziteka nyingi, lakini jemadari mmoja atakomesha ufidhuli wake na kurudisha ufidhuli wake juu yake. [19] [e]Baada ya hili atazigeukia ngome za nchi yake mwenyewe, lakini atajikwaa na kuanguka, wala hataonekana tena.

[20] [f]“Atakayetawala baada yake atamtuma mtoza ushuru ili kudumisha fahari ya kifalme. Hata hivyo, baada ya miaka michache ataangamizwa, lakini si katika hasira wala katika vita.

[21] [g]“Atakayetawala baada yake atakuwa mtu wa kudharauliwa ambaye hajapewa heshima ya kifalme. Atauvamia ufalme wakati watu wake wanapojiona wako salama, naye atautwaa kwa hila. [22] [h]Ndipo jeshi kubwa litafagiliwa mbele yake; jeshi pamoja na mkuu mmoja wa agano wataangamizwa. [23] [i]Baada ya kufanya mapatano naye, atatenda kwa udanganyifu, na akitumia watu wachache tu ataingia madarakani. [24] [j]Wakati majimbo yaliyo tajiri sana yanajiona salama, atayavamia, naye atafanikisha kile ambacho baba zake wala babu zake hawakuweza. Atagawa nyara, mateka na utajiri miongoni mwa wafuasi wake. Atafanya hila ya kupindua miji yenye maboma, lakini kwa muda mfupi tu.

[25] “Pamoja na jeshi kubwa atachochea nguvu zake na ushujaa wake dhidi ya mfalme wa Kusini. Mfalme wa Kusini atafanya vita na jeshi lenye nguvu sana, lakini hataweza kusimama kwa sababu ya kwa hila zilizofanywa dhidi yake. [26] Wale wanaokula kutoka kwenye ruzuku za mfalme watajaribu kumwangamiza; jeshi lake litafagiliwa mbali, nao wengi watakufa vitani. [27] [k]Wafalme hawa wawili, mioyo yao ikiwa imekusudia mabaya, wataketi kwenye meza moja na kudanganyana wao kwa wao, lakini pasipo faida, kwa sababu bado mwisho utakuja katika wakati ulioamriwa. [28] Mfalme wa Kaskazini atarudi katika nchi yake na utajiri mwingi, lakini atakuwa ameukaza moyo wake kinyume na agano takatifu. Atachukua hatua dhidi ya hilo agano, kisha atarudi nchi yake.

[29] “Wakati ulioamriwa, atavamia tena Kusini, lakini wakati huu matokeo yake yatakuwa tofauti na yale ya wakati wa kwanza. [30] [l]Meli za nchi ya Kitimu zitampinga, naye atavunjika moyo. Ndipo atarudi nyuma na kutoa wazi hasira yake dhidi ya agano takatifu. Atarudi na kuonyesha fadhili kwa wale waliachao agano takatifu.

---

[a]**11:15** Eze 4:2; Za 33:16
[b]**11:16** Dan 8:4-7, 9; Yos 1:5
[c]**11:17** Za 20:4; 2Nya 20:3
[d]**11:18** Isa 66:19; Yer 25:22; Hos 12:14
[e]**11:19** Za 27:2; 46:2; 37:36; Eze 26:21
[f]**11:20** Isa 60:17
[g]**11:21** Dan 4:17; 8:25; 2Sam 15:6
[h]**11:22** Dan 8:10-11; Isa 28:15
[i]**11:23** Dan 8:25
[j]**11:24** Neh 9:25
[k]**11:27** Za 64:6; 12:2; Yer 9:5; Hab 2:3
[l]**11:30** Hes 24:24; Mwa 10:4; 1Sam 17:32; Ay 15:13

31 [a]“Majeshi yake yenye silaha yatainuka
ili kunajisi ngome ya Hekalu, na kuondolea
mbali sadaka ya kuteketezwa ya kila siku.
Ndipo watalisimamisha chukizo la uharibifu
lisababishalo ukiwa. 32 [b]Kwa udanganyifu
atapotosha wale walionajisi agano, lakini
watu wanaomjua Mungu wao watampinga
kwa uthabiti.
33 [c]“Wenye hekima watawafundisha
wengi, ingawa kwa kitambo watauawa kwa
upanga au kuchomwa moto, au kukamatwa
au kufanywa mateka. 34 [d]Watakapoanguka,
watapokea msaada kidogo, nao wengi
ambao si waaminifu wataungana nao.
35 [e]Baadhi ya wenye hekima watajikwaa,
ili waweze kusafishwa, kutakaswa na
kufanywa wasio na waa mpaka wakati wa
mwisho, kwa maana bado litakuja kwa
wakati ulioamriwa.

*Mfalme Ajikwezaye Mwenyewe*

36 [f]“Mfalme atafanya apendavyo.
Atajikweza na kujitukuza juu ya kila
mungu, naye atasema mambo ambayo
hayajasikiwa dhidi ya Mungu wa miungu.
Atafanikiwa hadi wakati wa ghadhabu
utimie, kwa maana kile kilichokusudiwa
lazima kitokee. 37 Hataonyesha heshima
kwa miungu ya baba zake au kwa yule
aliyetamaniwa na wanawake, wala hatajali
mungu yeyote, bali atajikweza mwenyewe
juu yao wote. 38 Badala ya kuwajali miungu,
ataheshimu mungu wa ngome; mungu
ambaye hakujulikana na baba zake ndiye
atamheshimu kwa dhahabu na fedha, kwa
vito vya thamani na zawadi za thamani
kubwa. 39 Atashambulia ngome zenye nguvu
mno kwa msaada wa mungu wa kigeni naye
atawaheshimu sana wale watakaomkubali
yeye. Atawafanya watawala juu ya watu
wengi, na atagawa nchi kwa gharama.
40 [g]“Katika wakati wa mwisho, mfalme wa
Kusini atapigana naye vita, naye mfalme
wa Kaskazini atamshambulia kwa magari
ya vita, askari wapanda farasi, na idadi
kubwa ya meli. Atavamia nchi nyingi
na kuzikumba nchi hizo kama mafuriko.
41 [h]Pia ataivamia Nchi ya Kupendeza. Nchi
nyingi zitapinduliwa, bali Edomu, Moabu
na viongozi wa Amoni wataokolewa kutoka
mkono wake. 42 Atapanua mamlaka yake
juu ya nchi nyingi; hata Misri haitaepuka.
43 [i]Atamiliki hazina za dhahabu, fedha na
utajiri wote wa Misri, pamoja na Walibia na
Wakushi kwa kujisalimisha. 44 Lakini taarifa
kutoka mashariki na kaskazini zitamshtua,
naye ataondoka kwa ghadhabu nyingi ili
kuangamiza na kuharibu kabisa wengi.
45 [j]Atasimika hema zake za ufalme kati ya
bahari na mlima mtakatifu wa kupendeza.
Hata hivyo, atafikia mwisho wake, wala
hakuna yeyote atakayemsaidia.

*Nyakati Za Mwisho*

12 [k]“Katika wakati huo Mikaeli, mtawala
mkuu ambaye huwalinda watu wako,
atainuka. Kutakuwako wakati wa taabu
ambao haujatokea tangu mwanzo wa
mataifa hadi wakati huo. Lakini wakati
huo, watu wako, kila mmoja ambaye jina
lake litakutwa limeandikwa kwenye kitabu,
ataokolewa. 2 [l]Wengi ambao wamelala
kwenye mavumbi wataamka, baadhi yao
kwa uzima wa milele, wengine kwa aibu
na kudharauliwa milele. 3 [m]Wale wenye
hekima watang’aa kama mwanga wa
mbingu, nao wale ambao huwaongoza

[a]**11:31** Yer 19:4; Mt 24:15; Hos 3:4; Dan 8:11-13; 9:27; Mk 13:14
[b]**11:32** 1Nya 28:9; Mik 5:7-9
[c]**11:33** Dan 12:3; Mal 2:7; Yn 16:2; Ebr 11:32-38; Mt 24:9
[d]**11:34** Mt 7:15; Rum 16:18
[e]**11:35** Ay 28:1; Yn 15:2; Za 78:38; Isa 48:10; Dan 12:10; Zek 13:9
[f]**11:36** 1The 2:4; Ufu 13:5-6; Kum 10:17; Isa 26:20; Yud 16; Dan 7:25; Isa 10:25
[g]**11:40** Isa 21:1; 5:28; Eze 38:4; Isa 8:7
[h]**11:41** Isa 11:14; Yer 48:47; Mal 3:12; Eze 20:6
[i]**11:43** Eze 30:4; 2Nya 12:3; Nah 3:9
[j]**11:45** Isa 2:2-4; Dan 8:9
[k]**12:1** Dan 10:13; Yud 9; Dan 9:12; Lk 10:20; Yer 17:13; Mt 24:21; Mk 13:19; Yer 30:7; Za 56:8; Kut 32:32
[l]**12:2** Isa 26:19; Yn 5:28-29; Mt 25:46; Yn 11:24
[m]**12:3** Dan 11:33; Yn 5:35; Flp 2:15; Mit 4:18; 1Kor 15:42; Mt 13:43

wengi kutenda haki, watang'aa kama nyota
milele na milele. 4 [a]Lakini wewe Danieli,
yafunge na kuyatia muhuri maneno ya
kitabu hiki mpaka wakati wa mwisho.
Wengi watakwenda huku na huko, na
maarifa yataongezeka."
5 [b]Ndipo mimi Danieli nikaangalia, nako
mbele yangu walisimama wengine wawili,
mmoja katika ukingo huu wa mto, na
mwingine ukingo wa pili wa mto. 6 [c]Mmoja
wao akasema na yule mtu aliyevaa nguo za
kitani, aliyekuwa juu ya maji ya mto, "Je,
itachukua muda gani kabla mambo haya
ya kushangaza hayajatimizwa?"
7 [d]Kisha mtu yule aliyevaa nguo za
kitani, aliyekuwa juu ya maji ya mto,
akainua mkono wake wa kuume na mkono
wake wa kushoto kuelekea mbinguni,
nami nikamsikia akiapa kwa jina lake
yeye aishiye milele, akisema, "Itakuwa
wakati, nyakati mbili, na nusu wakati.[e]
Nguvu za watu watakatifu zitakapokuwa
zimevunjwa kabisa, ndipo mambo haya
yote yatakapotimizwa."
8 Nilisikia, lakini sikuelewa. Kwa hiyo
nikauliza, "Bwana wangu, matokeo ya haya
yote yatakuwa nini?"
9 [f]Akajibu, "Danieli, enenda zako, kwa
sababu maneno haya yamefungwa na
kutiwa muhuri mpaka wakati wa mwisho.
10 [g]Wengi watatakaswa, na kuondolewa
mawaa na kufanywa safi, lakini waovu
wataendelea kuwa waovu. Hakuna mmoja
wa waovu atakayefahamu, lakini wale
wenye hekima watafahamu.
11 [h]"Tangu wakati ule wa kukomeshwa
dhabihu ya kila siku na kusimamishwa
kwa chukizo la uharibifu, kutakuwako
siku 1,290. 12 [i]Amebarikiwa mtu yule
atakayevumilia hadi kufikia mwisho wa
hizo siku 1,335.
13 [j]"Lakini wewe, enenda zako mpaka
mwisho. Utapumzika, nawe ndipo mwisho
wa hizo siku utafufuka ili kuupokea urithi
uliowekewa."

[a]**12:4** Isa 8:16; Ufu 22:10; Yer 5:1
[b]**12:5** Dan 10:4
[c]**12:6** Eze 9:2; Dan 8:13; Za 74:9
[d]**12:7** Dan 6:26; Ufu 10:5-7; Lk 21:24; Dan 8:24; 8:24; Ufu 11:2; Mwa 14:22
[e]7 Wakati, nyakati mbili na nusu wakati maana yake mwaka mmoja, miaka miwili, na nusu mwaka, yaani miaka mitatu na nusu.
[f]**12:9** Isa 29:11
[g]**12:10** Isa 1:25; Zek 13:9; Hos 14:9; Isa 32:7; Ufu 22:11; Dan 11:35
[h]**12:11** Mk 13:14; Dan 8:11; 9:27; Mt 24:15; Kut 29:38; Ufu 11:2
[i]**12:12** Isa 30:18; Eze 4:5-6; Dan 8:14
[j]**12:13** Isa 57:2

# HOSEA

1 [a]Neno la BWANA lililomjia Hosea mwana
wa Beeri wakati wa utawala wa Uzia,
Yothamu, Ahazi na Hezekia, wafalme wa
Yuda, na wakati wa utawala wa Yeroboamu
mwana wa Yehoashi, mfalme wa Israeli.

*Mke Wa Hosea Na Watoto*

2 [b]Wakati BWANA alipoanza kuzungumza
kupitia Hosea, BWANA alimwambia, “Nenda
ukajitwalie mwanamke wa uzinzi na watoto
wa uzinzi, kwa sababu nchi ina hatia ya
uzinzi wa kupindukia kwa kumwacha
BWANA.” 3 [c]Kwa hiyo alimwoa Gomeri
binti Diblaimu, naye akachukua mimba
na kumzalia Hosea mwana.

4 [d]Kisha BWANA akamwambia Hosea,
“Mwite Yezreeli,[e] kwa kuwa kitambo kidogo
nitaiadhibu nyumba ya Yehu kwa ajili ya
mauaji ya kule Yezreeli, nami nitaukomesha
ufalme wa Israeli. 5 [f]Katika siku ile nitavunja
upinde wa Israeli katika Bonde la Yezreeli.”

6 [g]Gomeri akachukua tena mimba
akamzaa binti. Kisha BWANA akamwambia
Hosea, “Mwite Lo-Ruhama,[h] kwa maana
sitaonyesha tena upendo kwa nyumba ya
Israeli, kwamba nisije kabisa nikawasamehe.
7 [i]Hata hivyo nitaonyesha upendo kwa
nyumba ya Yuda, nami nitawaokoa si kwa
upinde, upanga au vita, wala kwa farasi na
wapanda farasi, bali kwa njia ya BWANA
Mungu wao.”

8 Baada ya Gomeri kumwachisha
Lo-Ruhama kunyonya, Gomeri alipata
mwana mwingine. 9 [j]Kisha BWANA akasema,
“Mwite Lo-Ami[k] kwa maana ninyi si watu
wangu, nami si Mungu wenu.

10 [l]“Hata hivyo Waisraeli watakuwa kama
mchanga kando ya bahari, ambao hauwezi
kupimika wala kuhesabiwa. Mahali pale
walipoambiwa, ‘Ninyi si watu wangu,’
wao wataitwa ‘wana wa Mungu aliye
hai.’ 11 [m]Watu wa Yuda na watu wa Israeli
wataunganishwa tena, nao watamchagua
kiongozi mmoja nao watakwea watoke
katika nchi, kwa kuwa siku ya Yezreeli
itakuwa kuu sana.

2 [n]“Waambie ndugu zako, ‘Watu wangu,’
na pia waambie dada zako, ‘Wapendwa
wangu.’

*Israeli Aadhibiwa Na Kurudishwa*

2 [o]“Mkemeeni mama yenu, mkemeeni,
kwa maana yeye si mke wangu,
nami si mume wake.
Aondoe sura ya uzinzi katika uso
wake
na uzinzi kati ya matiti yake.
3 [p]Kama sivyo nitamvua nguo zake
awe uchi
na kumwacha uchi kama siku ile
aliyozaliwa.
Nitamfanya kama jangwa,
nitamgeuza awe nchi ya kiu,
nami nitamuua kwa kiu.
4 [q]Sitaonyesha upendo wangu kwa
watoto wake,
kwa sababu ni watoto wa uzinzi.
5 [r]Mama yao amekosa uaminifu
na amewachukua mimba katika
aibu.

[a]**1:1** Mik 1:1; Isa 1:1; 2Fal 13:13; 14:12; 1Nya 3:12-13; Yer 1:2; 2Fal 14:21
[b]**1:2** Amu 2:17; Yer 3:14; Hos 2:5; 3:1; Yer 3:1; Kum 31:16
[c]**1:3** Hos 1:6
[d]**1:4** 1Sam 29:1; 1Fal 18:45; 2Fal 10:1-14; Hos 2:22
[e]4 Yezreeli maana yake Mungu hupanda.
[f]**1:5** Yos 15:56; 1Sam 29:1; 2Fal 15:29
[g]**1:6** Hos 2:4, 23; 1:6
[h]6 Lo-Ruhama maana yake Sio mpenzi wangu.
[i]**1:7** Za 44:6; Zek 2:6
[j]**1:9** Eze 11:19-20; 1Pet 2:10
[k]9 Lo-Ami maana yake Sio watu wangu.
[l]**1:10** Mwa 22:17; Yer 33:22; Rum 9:26; Hos 2:23; Hes 23:10; Yos 3:10
[m]**1:11** Isa 11:12-13; Yer 23:5-8; 30:9; Eze 37:15-28
[n]**2:1** 1Pet 2:10; Hos 2:5
[o]**2:2** Isa 1:21; 50:1; Eze 16:25; 23:45; Hos 4:5
[p]**2:3** Eze 16:4, 37; 19:13; Isa 32:13-14
[q]**2:4** Eze 8:18; Hos 1:6; 5:7
[r]**2:5** Yer 3:6; 44:17-18; Hos 1:2

Gomeri alisema, ‘Nitawaendea
wapenzi wangu,
ambao hunipa chakula changu
na maji yangu,
sufu yangu na kitani yangu, mafuta
yangu
na kinywaji changu.’
6 [a]Kwa hiyo mimi Mungu nitaizuia
njia yake
kwa vichaka vya miiba,
nitamjengea ukuta ili kwamba
asiweze kutoka.
7 [b]Gomeri atawafuatia wapenzi wake
lakini hatawapata;
atawatafuta lakini hatawapata.
Kisha atasema,
‘Nitarudi kwa mume wangu kama
kwanza,
kwa maana nilikuwa na hali njema
zaidi
kuliko sasa.’
8 [c]Gomeri hajakubali kuwa mimi ndiye
niliyempa nafaka, divai mpya na
mafuta,
niliyemwongezea fedha na dhahabu
waliyoitumia
kwa kumtumikia Baali.

9 [d]“Kwa hiyo nitachukua nafaka yangu
wakati itakapokomaa
na divai yangu mpya wakati
itakapokuwa tayari.
Nitamnyang’anya sufu yangu na
kitani yangu
iliyokusudiwa kufunika uchi wake.
10 [e]Basi sasa nitaufunua ufisadi wake
mbele ya wapenzi wake;
hakuna yeyote atakayemtoa
mikononi mwangu.
11 [f]Nitakomesha furaha na macheko
yake yote:
sikukuu zake za mwaka,
sikukuu za Miandamo ya Mwezi,
siku zake za Sabato,
sikukuu zake zote zilizoamriwa.
12 [g]Nitaiharibu mizabibu yake na mitini
yake,
ambayo alisema yalikuwa malipo
yake
kutoka kwa wapenzi wake;
nitaifanya kuwa kichaka,
nao wanyama pori wataila.
13 [h]Nitamwadhibu kwa ajili ya siku
alizowafukizia uvumba Mabaali;
alipojipamba kwa pete
na kwa vito vya thamani,
na kuwaendea wapenzi wake,
lakini mimi alinisahau,”
asema Bwana.

14 [i]“Kwa hiyo sasa nitamshawishi;
nitamwongoza hadi jangwani
na kuzungumza naye kwa upole.
15 [j]Huko nitamrudishia mashamba yake
ya mizabibu,
nami nitalifanya Bonde la Akori[k]
mlango wa matumaini.
Huko ataimba kama alivyofanya
katika siku za ujana wake,
kama siku zile alizotoka Misri.

16 [l]“Katika siku ile,” asema Bwana,
“utaniita mimi ‘Mume wangu’;
hutaniita tena mimi ‘Bwana
wangu.’
17 [m]Nitaondoa majina ya Mabaali
kutoka midomoni mwake,
wala hataomba tena kwa majina
yao.

[a]**2:6** Ay 3:23; 19:8; Mao 3:9
[b]**2:7** Hos 5:13; Yer 3:1; Eze 16:8; Isa 54:5
[c]**2:8** Eze 16:15-19; Hes 18:12; Kum 8:18; Hos 8:4
[d]**2:9** Hos 8:7; 9:2
[e]**2:10** Eze 16:37; 23:10; Yer 13:26
[f]**2:11** Isa 1:14; 24:8; Amo 5:21; 8:10; Yer 7:34; 16:9; Hos 9:5
[g]**2:12** Isa 5:6; 7:23; Yer 8:13; Hos 5:7; 13:8
[h]**2:13** Yer 7:9; Hos 4:13; 8:14; 11:2; 13:6; Eze 16:17; 23:40; Isa 65:7
[i]**2:14** Eze 19:14
[j]**2:15** Yos 7:24-26; Kut 15:1-18; Eze 16:22; 28:26; Hos 12:9; 1Kor 13:13
[k]15 Akori maana yake ni Taabu.
[l]**2:16** Isa 54:5
[m]**2:17** Kut 23:13; Za 16:4; Yer 23:7; Zek 13:2

18 [a]Katika siku ile nitafanya Agano kwa ajili yao
na wanyama wa kondeni, na ndege wa angani,
na viumbe vile vitambaavyo ardhini.
Upinde, upanga na vita,
nitaondolea mbali katika nchi,
ili kwamba wote waweze kukaa salama.
19 [b]Nitakuposa uwe wangu milele;
nitakuposa kwa uadilifu na haki,
kwa upendo na huruma.
20 [c]Nitakuposa kwa uaminifu,
nawe utamkubali BWANA.

21 [d]"Katika siku ile nitajibu,"
asema BWANA,
"nitajibu kwa anga,
nazo anga zitajibu kwa nchi;
22 [e]nayo nchi itajibu kwa nafaka,
divai mpya na mafuta,
navyo vitajibu kwa Yezreeli.
23 [f]Nitampanda katika nchi kwa ajili yangu mwenyewe;
nami nitaonyesha pendo langu kwake
yule ambaye nilimwita, 'Si mpenzi wangu.[g]'
Nitawaambia wale walioitwa, 'Sio watu wangu,'[h]
'Ninyi ni watu wangu';
nao watasema, 'Wewe ndiwe Mungu wangu.' "

*Upatanisho Wa Hosea Na Mkewe*

3 [i]BWANA akaniambia, "Nenda, ukaonyeshe upendo wako kwa mke wako tena, ingawa amependwa na mwingine naye
ni mzinzi. Mpende kama BWANA apendavyo Waisraeli, ingawa wanageukia miungu mingine na kupenda mikate mitamu ya zabibu kavu iliyowekwa wakfu."
2 Basi nilimnunua huyo mwanamke kwa shekeli kumi na tano[j] za fedha, pia kwa kiasi kama cha homeri moja na nusu[k] ya shayiri.
3 [l]Kisha nilimwambia, "Utaishi nami kwa siku nyingi, hupaswi kuwa kahaba au kuwa na uhusiano wa karibu na mtu yeyote, nami nitaishi na wewe."
4 [m]Kwa maana Waisraeli wataishi siku nyingi bila kuwa na mfalme wala mkuu, bila kuwa na dhabihu wala mawe matakatifu, bila kisibau wala sanamu.
5 [n]Baadaye Waisraeli watarudi na kumtafuta BWANA Mungu wao na Daudi mfalme wao. Watakuja wakitetemeka kwa BWANA na kwa baraka zake katika siku za mwisho.

*Shtaka Dhidi Ya Israeli*

4 [o]Sikieni neno la BWANA, enyi Waisraeli,
kwa sababu BWANA analo shtaka
dhidi yenu ninyi mnaoishi katika nchi:
"Hakuna uaminifu, hakuna upendo,
hakuna kumjua Mungu katika nchi.
2 [p]Kuna kulaani tu, uongo na uuaji,
wizi na uzinzi,
bila kuwa na mipaka,
nao umwagaji damu mmoja baada ya mwingine.

[a]**2:18** Ay 5:22-23; Za 49:6; Zek 9:10; Eze 34:25; Yer 23:6
[b]**2:19** Isa 1:27; 62:4; 54:8; 2Kor 11:2
[c]**2:20** Yer 31:34; Hos 4:1; 6:6; 13:4; Eze 16:8
[d]**2:21** Zek 8:12; Mal 3:10-11; Isa 55:10
[e]**2:22** Yer 31:12; Yoe 2:19; Hos 14:7; Eze 36:29-30
[f]**2:23** Yer 29:12; 31:27; Isa 19:25; Hos 1:10; Rum 9:25; Zek 13:9; 1Pet 2:10
[g]23 Kiebrania ni Lo-Ruhama.
[h]23 Kiebrania ni Lo-Ami.
[i]**3:1** Hos 1:2; 2Sam 6:19
[j]2 Shekeli 15 za fedha ni sawa na gramu 170.
[k]2 Homeri moja na nusu ni kama lita 330.
[l]**3:3** Kum 21:23
[m]**3:4** Hos 2:11; 13:11; Dan 11:31; Amu 18:14-17, 23-24; Mao 2:9; Kum 28:6; Zek 10:2; Kut 25:7
[n]**3:5** 1Sam 13:14; Eze 34:23-24; Kum 4:30; Yer 50:4-5; Isa 9:13; 10:20; Hos 5:15; Mik 4:1-2; Za 18:45
[o]**4:1** Mit 10:21; 24:2; Mik 6:2; Isa 1:3; Ay 10:2; Yer 2:9; 7:28; 51:5; Hos 2:20
[p]**4:2** Isa 59:3; Hos 5:2; 6:2; 7:1; 11:12; Eze 22:2-9; 1Fal 21:16

3 [a]Kwa sababu hii nchi huomboleza,
wote waishio ndani mwake wanadhoofika,
wanyama wa kondeni, ndege wa angani
na samaki wa baharini wanakufa.

4 [b]"Lakini mtu awaye yote na asilete shtaka,
mtu yeyote na asimlaumu mwenzake,
kwa maana watu wako ni kama wale
waletao mashtaka dhidi ya kuhani.
5 [c]Unajikwaa usiku na mchana,
nao manabii hujikwaa pamoja nawe.
Kwa hiyo nitamwangamiza mama yako:
6 [d]watu wangu wanaangamizwa
kwa kukosa maarifa,

"Kwa kuwa wewe umeyakataa maarifa,
mimi nami nitakukataa wewe
usiwe kuhani kwangu mimi;
kwa kuwa umeacha kuijali sheria ya Mungu wako
mimi nami sitawajali watoto wako.
7 [e]Kadiri makuhani walivyoongezeka,
ndivyo walivyozidi kutenda dhambi dhidi yangu,
walibadilisha utukufu wao kwa kitu cha aibu.
8 [f]Hujilisha dhambi za watu wangu
na kupendezwa na uovu wao.
9 [g]Hata itakuwa: Kama walivyo watu,
ndivyo walivyo makuhani.
Nitawaadhibu wote wawili kwa ajili ya njia zao
na kuwalipa kwa matendo yao.

10 [h]"Watakula lakini hawatashiba;
watajiingiza katika ukahaba
lakini hawataongezeka,
kwa sababu wamemwacha BWANA
na kujiingiza wenyewe
11 [i]katika ukahaba,
divai ya zamani na divai mpya,
ambavyo huondoa ufahamu
12 [j]wa watu wangu.
Hutaka shauri kutoka kwa sanamu ya mti
nao hujibiwa na fimbo ya mti.
Roho ya ukahaba imewapotosha,
hawana uaminifu kwa Mungu wao.
13 [k]Wanatoa dhabihu juu ya vilele vya milima
na sadaka za kuteketezwa juu ya vilima,
chini ya mialoni, milibua na miela,
ambako kuna vivuli vizuri.
Kwa hiyo binti zenu wamegeukia ukahaba
na wake za wana wenu uzinzi.

14 [l]"Sitawaadhibu binti zenu wakati
wanapogeukia ukahaba,
wala wake za wana wenu
wanapofanya uzinzi,
kwa sababu wanaume wenyewe huandamana na malaya
na kutambikia pamoja na makahaba
wa mahali pa kuabudia miungu:
watu wasiokuwa na ufahamu
wataangamia!

15 [m]"Ingawa umefanya uzinzi, ee Israeli,
Yuda naye asije akawa na hatia.

---

[a]**4:3** Yer 4:25, 28; 9:10; Amo 8:8; Isa 15:6; 33:9; Sef 1:3
[b]**4:4** Kum 17:12; Eze 3:26
[c]**4:5** Eze 7:19; 14:7; Hos 2:2
[d]**4:6** Mit 10:21; Hos 2:13; 8:1-12; Mal 2:7-8
[e]**4:7** Hab 2:16; Hos 9:11; 13:6
[f]**4:8** Isa 56:11; Mik 3:11; Hos 14:1
[g]**4:9** Isa 24:2; Yer 5:31; Hos 8:13; 10:10; 12:2
[h]**4:10** Mik 6:14; Isa 55:2; Hos 7:14; 9:17; Eze 22:9; Law 26:26
[i]**4:11** Isa 28:7; Hos 5:4; Mit 20:1; Law 10:9; 1Sam 25:36
[j]**4:12** Yer 2:27; Ufu 17:2; Hab 2:19; Isa 44:20; Hes 15:39; Za 73:27
[k]**4:13** Isa 1:28; Hos 2:13; 10:9; Yer 2:20; Amo 7:17; Rum 1:28
[l]**4:14** Mwa 38:21; Hos 9:10; Mit 10:21
[m]**4:15** Hos 9:15; 12:11; Amo 4:4; Yos 7:2

"Usiende Gilgali,
usipande kwenda Beth-Aveni[a]
Wala usiape,
'Hakika kama BWANA aishivyo!'
16 [b]Waisraeli ni wakaidi,
kama mtamba wa ng'ombe
ambaye ni mkaidi.
Ni jinsi gani basi BWANA anaweza
kuwachunga
kama wana-kondoo
katika shamba la majani?
17 [c]Efraimu amejiunga na sanamu,
ondokana naye!
18 [d]Hata wakati wamemaliza vileo vyao
wanaendelea na ukahaba wao,
watawala wao hupenda sana
njia za aibu.
19 [e]Kisulisuli kitawafagilia mbali
na dhabihu zao zitawaletea aibu.

*Hukumu Dhidi Ya Israeli*

5 [f]"Sikieni hili, enyi makuhani!
Kuweni wasikivu, enyi
Waisraeli!
Sikieni, ee nyumba ya mfalme!
Hukumu hii ni dhidi yenu:
Mmekuwa mtego huko Mispa,
wavu uliotandwa juu ya Tabori.
2 [g]Waasi wamezidisha sana mauaji.
Mimi nitawatiisha wote.
3 [h]Ninajua yote kuhusu Efraimu,
Israeli hukufichika kwangu.
Efraimu, sasa umegeukia ukahaba,
Israeli amenajisika.

4 [i]"Matendo yao hayawaachii
kurudi kwa Mungu wao.
Roho ya ukahaba imo ndani ya
mioyo yao,
hawamkubali BWANA.
5 [j]Kiburi cha Israeli kinashuhudia
dhidi yao;
Waisraeli, hata Efraimu,
wanajikwaa katika dhambi zao;
pia Yuda atajikwaa pamoja nao.
6 [k]Wakati wanapokwenda na makundi
yao
ya kondoo na ng'ombe
kumtafuta BWANA,
hawatampata;
yeye amejiondoa kutoka kwao.
7 [l]Wao si waaminifu kwa BWANA;
wamezaa watoto haramu.
Sasa sikukuu zao za Mwandamo wa
Mwezi
zitawaangamiza wao
pamoja na mashamba yao.

8 [m]"Pigeni tarumbeta huko Gibea,
baragumu huko Rama.
Paza kilio cha vita huko Beth-Aveni,[n]
ongoza, ee Benyamini.
9 [o]Efraimu ataachwa ukiwa
katika siku ya kuadhibiwa.
Miongoni mwa makabila ya Israeli
ninatangaza lile ambalo halina
budi kutukia.
10 [p]Viongozi wa Yuda ni kama wale
wanaosogeza mawe ya mpaka.
Nitamwaga ghadhabu yangu juu yao
kama mafuriko ya maji.

---

[a]15 Beth-Aveni maana yake Nyumba ya Ubatili (au Uovu), jina lingine la Betheli kwa dhihaka.
[b]**4:16** Isa 5:17; 7:25; Kut 32:9; Yer 31:18
[c]**4:17** Mt 15:14
[d]**4:18** Mik 3:11; 7:3
[e]**4:19** Hos 12:11; 13:15; Isa 1:29
[f]**5:1** Hos 6:9; 9:8; Ay 10:12; Yer 5:26
[g]**5:2** Hos 4:2; 9:15
[h]**5:3** Eze 23:7; Za 90:8; Hos 1:2; 6:10; Amo 5:12
[i]**5:4** Hos 4:6, 11; 7:10; Yer 4:22
[j]**5:5** Isa 3:9; Yer 2:19; Hos 7:10
[k]**5:6** Mik 6:6-7; Mit 1:28; Mal 1:10; Eze 8:6; Isa 1:26
[l]**5:7** Isa 1:14; 24:16; Hos 2:4, 11-12; 6:7; Eze 12:28
[m]**5:8** Amu 19:12; Hos 4:15; 10:9; Isa 10:29; Yos 7:2; Hes 10:2; Yer 4:21
[n]8 Beth-Aveni maana yake Nyumba ya Ubatili (au Uovu), jina lingine la Betheli kwa dhihaka.
[o]**5:9** Isa 37:3; Hos 9:11-17; Isa 46:10; 7:16; Zek 1:6
[p]**5:10** Kum 19:14; Eze 7:8

11 [a]Efraimu ameonewa,
amekanyagwa katika hukumu
kwa kuwa amekusudia kufuatia
sanamu.
12 [b]Mimi ni kama nondo kwa Efraimu,
na kama uozo kwa watu wa Yuda.

13 [c]"Wakati Efraimu alipoona ugonjwa
wake,
naye Yuda vidonda vyake,
ndipo Efraimu alipogeukia Ashuru,
na kuomba msaada kwa mfalme
mkuu.
Lakini hawezi kukuponya,
wala hawezi kukuponya vidonda
vyako.
14 [d]Kwa maana nitakuwa kama simba
kwa Efraimu,
kama simba mkubwa kwa Yuda.
Nitawararua vipande vipande na
kuondoka;
nitawachukua mbali,
na hakuna wa kuwaokoa.
15 [e]Kisha nitarudi mahali pangu
mpaka watakapokubali kosa lao.
Nao watautafuta uso wangu;
katika taabu yao watanitafuta kwa
bidii."

*Israeli Asiye Na Toba*

6 [f]"Njooni, tumrudie BWANA.
Ameturarua vipande
vipande
lakini atatuponya;
ametujeruhi lakini
atatufunga majeraha yetu.
2 [g]Baada ya siku mbili atatufufua;
katika siku ya tatu atatuinua,
ili tuweze kuishi mbele zake.
3 [h]Tumkubali BWANA,
tukaze kumkubali yeye.
Kutokea kwake ni hakika kama vile
kuchomoza kwa jua;
atatujia kama mvua za masika,
kama vile mvua za vuli
ziinyweshavyo nchi."

4 [i]"Nifanye nini nawe, Efraimu?
Nifanye nini nawe, Yuda?
Upendo wako ni kama ukungu wa
asubuhi,
kama umande wa alfajiri
utowekao.
5 [j]Kwa hiyo ninawakata ninyi vipande
vipande
kwa kutumia manabii wangu;
nimewaua ninyi kwa maneno ya
kinywa changu,
hukumu zangu zinawaka
kama umeme juu yenu.
6 [k]Kwa maana nataka rehema, wala si
dhabihu,
kumkubali Mungu zaidi
kuliko sadaka za kuteketezwa.
7 [l]Wamevunja Agano kama Adamu:
huko hawakuwa waaminifu
kwangu.
8 [m]Gileadi ni mji wenye watu waovu,
umetiwa madoa kwa nyayo za
damu.
9 [n]Kama wanyang'anyi wamviziavyo
mtu,
ndivyo magenge ya makuhani
wafanyavyo;
wanaulia watu kwenye njia iendayo
Shekemu,
wakifanya uhalifu wa aibu.
10 [o]Nimeona jambo la kutisha
katika nyumba ya Israeli.

---

[a]**5:11** Hos 9:16; Mik 6:16
[b]**5:12** Ay 13:28; Isa 51:8; Ay 18:16
[c]**5:13** Hes 12:1; Eze 23:5; Mao 5:6; Hos 2:7; Yer 30:12; Isa 7:16; 3:7
[d]**5:14** Ay 10:16; Yer 4:7; Kum 32:39; Mik 5:8; Amo 3:4
[e]**5:15** Hes 21:7; Za 24:6; 50:15; Yer 2:27; Eze 20:43; Isa 18:4; 64:9
[f]**6:1** Ay 16:9; Kum 32:39; Mao 3:11; Ay 5:18; Isa 10:20; 19:22; Hes 12:13; Yer 3:22; 30:17; Hos 14:4
[g]**6:2** Mit 2:1-9; Za 80:18; 30:5; Mt 16:21
[h]**6:3** Ay 4:3; 29:23; Yoe 2:23; Hos 12:6; Za 72:6; Hos 11:10
[i]**6:4** Hos 11:8; 7:1; 13:3
[j]**6:5** Yer 5:14; 23:29; Ebr 4:12; Yer 1:9-10
[k]**6:6** 1Sam 15:22; Mk 12:33; Yer 4:22; Hos 2:20; Mit 21:3; Mt 12:7; Za 40:6
[l]**6:7** Mwa 9:11; Yer 11:10; Hos 5:7; 8:1
[m]**6:8** Hos 12:11
[n]**6:9** Yer 5:30-31; Eze 22:9; Za 10:8; Hos 4:2; Yer 7:9-10
[o]**6:10** Yer 5:31; Eze 23:7; Yer 23:14; Hos 5:3

Huko Efraimu amejitolea kwa
ukahaba
na Israeli amenajisika.

11 [a]“Pia kwa ajili yako, Yuda,
mavuno yameamriwa.

“Wakati wowote ningerejesha neema
ya watu wangu,

# 7

1 [b]kila mara nilipotaka kumponya
Israeli,
dhambi za Efraimu zinafichuliwa
na maovu ya Samaria
yanafunuliwa.
Wanafanya udanganyifu,
wevi huvunja nyumba,
maharamia hunyang’anya
barabarani,
2 [c]lakini hawafahamu kwamba
ninakumbuka matendo yao yote
mabaya.
Dhambi zao zimewameza,
ziko mbele zangu siku zote.

3 [d]“Wanamfurahisha sana mfalme kwa
maovu yao,
wakuu wao kwa uongo wao.
4 [e]Wote ni wazinzi,
wanawaka kama tanuru
ambayo moto wake mwokaji hana
haja ya kuuchochea
kuanzia kukanda unga
hadi umekwisha kuumuka.
5 [f]Katika sikukuu ya mfalme wetu
wakuu wanawaka kwa mvinyo,
naye anawaunga mkono wenye
mizaha.
6 [g]Mioyo yao ni kama tanuru,
wanamwendea kwa hila.
Hasira yao inafoka moshi usiku
kucha,
wakati wa asubuhi inalipuka
kama miali ya moto.
7 [h]Wote ni moto kama tanuru;
wanawaangamiza watawala wao.
Wafalme wake wote wanaanguka,
wala hakuna yeyote kati yao
aniitaye mimi.

8 [i]“Efraimu anajichanganya na
mataifa;
Efraimu ni mkate ambao
haukuiva.
9 [j]Wageni wananyonya nguvu zake,
lakini hafahamu hilo.
Nywele zake zina mvi hapa na pale,
lakini hana habari.
10 [k]Kiburi cha Israeli kinashuhudia
dhidi yake,
lakini pamoja na haya yote
harudi kwa BWANA Mungu wake
wala kumtafuta.

11 [l]“Efraimu ni kama hua,
hudanganywa kwa urahisi na hana
akili:
mara anaita Misri,
mara anageukia Ashuru.
12 [m]Wakati watakapokwenda,
nitatupa wavu wangu juu yao;
nitawavuta chini waanguke
kama ndege wa angani.
Nitakaposikia wakikusanyika
pamoja,
nitawanasa.
13 [n]Ole wao, kwa sababu
wamepotoka kutoka kwangu!
Maangamizi ni yao
kwa sababu wameniasi!

---

[a]**6:11** Yoe 3:12-13; Yer 51:33
[b]**7:1** Eze 24:13; Hos 4:2; 6:4; Kut 22:2; Sef 2:7; Za 126:1
[c]**7:2** Yer 14:10; 44:21; Mit 5:22; Yer 2:19; 4:18; Hos 8:13; Ay 35:15
[d]**7:3** Rum 1:32; Yer 28:1-4; Mik 7:3; Hos 4:2; 10:13
[e]**7:4** Yer 9:2
[f]**7:5** Isa 28:1, 7; Za 1:1
[g]**7:6** Za 21:9
[h]**7:7** Za 14:4; Sef 1:6; Isa 9:13; Hos 13:10
[i]**7:8** Za 106:35; Hos 5:13; 7:11
[j]**7:9** Isa 1:7; Hos 8:7
[k]**7:10** Hos 5:5; Isa 9:13
[l]**7:11** Mwa 8:8; Hos 9:3; 11:11; Mao 5:6; Yer 2:18
[m]**7:12** Eze 12:13; 32:3; Law 26:14
[n]**7:13** Hos 9:12, 17; Yer 14:10; 51:9; Eze 34:4-6; Mt 23:37; Za 116:11

Ninatamani kuwakomboa,
lakini wanasema uongo dhidi yangu.
14 [a]Hawanililii mimi kutoka mioyoni mwao,
bali wanaomboleza vitandani mwao.
Hukusanyika pamoja kwa ajili ya nafaka na divai mpya,
lakini hugeukia mbali nami.
15 [b]Niliwafundisha na kuwatia nguvu,
lakini wanapanga mabaya dhidi yangu.
16 [c]Hawamgeukii Yeye Aliye Juu Sana,
wako kama upinde wenye kasoro.
Viongozi wao wataanguka kwa upanga
kwa sababu ya maneno yao ya jeuri.
Kwa ajili ya hili watadhihakiwa
katika nchi ya Misri.

*Israeli Kuvuna Kisulisuli*

8 [d]"Wekeni tarumbeta midomoni mwenu!
Tai yuko juu ya nyumba ya BWANA
kwa sababu watu wamevunja Agano langu,
wameasi dhidi ya sheria yangu.
2 [e]Israeli ananililia,
'Ee Mungu wetu, tunakukubali!'
3 [f]Lakini Israeli amekataa lile lililo jema,
adui atamfuatia.
4 [g]Wanaweka wafalme bila idhini yangu,
wamechagua wakuu bila kibali changu.
Kwa fedha zao na dhahabu
wamejitengenezea sanamu kwa ajili
ya maangamizi yao wenyewe.
5 [h]Ee Samaria, tupilieni mbali sanamu yenu ya ndama!
Hasira yangu inawaka dhidi yao.
Watakuwa najisi mpaka lini?
6 [i]Zimetoka katika Israeli!
Ndama huyu: ametengenezwa na fundi, si Mungu.
Atavunjwa vipande vipande,
yule ndama wa Samaria.

7 [j]"Wanapanda upepo
na kuvuna upepo wa kisulisuli.
Bua halina suke,
halitatoa unga.
Kama lingetoa nafaka,
wageni wangeila yote.
8 [k]Israeli amemezwa;
sasa yupo miongoni mwa mataifa
kama kitu kisicho na thamani.
9 [l]Kwa kuwa wamepanda kwenda Ashuru
kama punda-mwitu
anayetangatanga peke yake.
Efraimu amejiuza mwenyewe
kwa wapenzi.
10 [m]Ingawa wamejiuza wenyewe miongoni mwa mataifa,
sasa nitawakusanya pamoja.
Wataanza kudhoofika chini ya uonevu
wa mfalme mwenye nguvu.

11 [n]"Ingawa Efraimu alijenga madhabahu nyingi
kwa ajili ya sadaka za dhambi,
hizi zimekuwa madhabahu
za kufanyia dhambi.

[a]**7:14** Ay 35:9; Yer 3:10; Hos 4:10; 13:16; Za 78:34-37; Amo 2:8
[b]**7:15** Za 2:1; 140:2; Nah 1:9; Hos 11:3
[c]**7:16** Za 78:57; Eze 23:32; Hos 9:3; 11:5; Mal 3:14
[d]**8:1** Kum 28:49; Yer 4:13; 11:10; Hos 4:6; 6:7; Hes 10:2; Eze 33:3
[e]**8:2** Za 78:34; Mt 7:21
[f]**8:3** Mt 7:23; Tit 1:16
[g]**8:4** Hos 2:8; 13:1-2, 10; Mt 7:21; 1Fal 12:16-20; 2Fal 15:13, 17, 25
[h]**8:5** Hos 10:5; Yer 13:27; Hos 8:6
[i]**8:6** Yer 16:20; Hos 14:3; Kut 32:4
[j]**8:7** Ay 4:8; Gal 6:8; Hos 2:9; 7:9; 10:11-12; Mit 22:8; Isa 17:11; 66:15
[k]**8:8** Yer 22:28; 51:34; 2Fal 17:6; Yer 22:28; 48:38
[l]**8:9** Yer 2:18; 22:20; Mwa 16:12; Eze 23:5; Hos 5:13
[m]**8:10** Eze 16:37; 22:20; Yer 42:2; Dan 2:34
[n]**8:11** Hos 10:1; 12:11

12 [a]Nimeandika kwa ajili yao mambo mengi
kuhusu sheria yangu,
lakini wameziangalia
kama kitu cha kigeni.
13 [b]Wanatoa dhabihu nilizopewa mimi
nao wanakula hiyo nyama,
lakini BWANA hapendezwi nao.
Sasa ataukumbuka uovu wao
na kuadhibu dhambi zao:
Watarudi Misri.
14 [c]Israeli amemsahau Muumba wake
na kujenga majumba ya kifalme,
Yuda amejengea miji mingi ngome.
Lakini nitatuma moto kwenye miji yao
utakaoteketeza ngome zao."

*Adhabu Kwa Israeli*

9 [d]Usifurahie, ee Israeli;
usishangilie kama mataifa mengine.
Kwa kuwa hukuwa
mwaminifu kwa Mungu wako;
umependa ujira wa kahaba kwenye kila sakafu
ya kupuria nafaka.
2 [e]Sakafu za kupuria nafaka na mashinikizo ya kukamulia divai
havitalisha watu,
divai mpya itawapungukia.
3 [f]Hawataishi katika nchi ya BWANA,
Efraimu atarudi Misri
na atakula chakula
kilicho najisi huko Ashuru.
4 [g]Hawatammiminia BWANA sadaka ya divai
wala dhabihu zao hazitampendeza.
Dhabihu kama hizo zitakuwa kwao
kama mkate wa waombolezaji;
nao wote wazilao watakuwa najisi.
Chakula hiki kitakuwa kwa ajili yao wenyewe;
kisije katika Hekalu la BWANA.

5 [h]Mtafanya nini katika siku ya sikukuu zenu zilizoamriwa,
katika siku za sikukuu za BWANA?
6 [i]Hata ikiwa wataokoka maangamizi,
Misri atawakusanya,
nayo Memfisi[j] itawazika.
Hazina zao za fedha zitasongwa na michongoma,
nayo miiba itafunika mahema yao.
7 [k]Siku za adhabu zinakuja,
siku za malipo zimewadia.
Israeli na afahamu hili.
Kwa sababu dhambi zenu ni nyingi sana
na uadui wenu ni mkubwa sana,
nabii anadhaniwa ni mpumbavu,
mtu aliyeongozwa na Mungu
anaonekana mwendawazimu.
8 [l]Nabii, pamoja na Mungu wangu,
ndiye mlinzi juu ya Efraimu,
hata hivyo mitego inamngojea
katika mapito yake yote,
na uadui katika nyumba ya Mungu wake.
9 [m]Wamezama sana katika rushwa,
kama katika siku za Gibea.

[a]**8:12** Hos 8:1; Kum 4:6; Za 119:18; 147:19-20
[b]**8:13** Yer 6:20; 7:21; Neh 9:13-14; Hos 4:9; 9:3-9; Ay 21:14
[c]**8:14** Kum 32:18; Isa 17:10; Yer 5:17; Amo 2:5; 1Fal 12:31; Hos 2:13; Za 95:6
[d]**9:1** Isa 22:12-13; 24:16; Za 73:27; Hos 7:14; 10:5; Mwa 30:15
[e]**9:2** Isa 24:7; Yoe 1:10; Hos 2:9
[f]**9:3** Kum 4:26-27; Amo 7:17; Eze 4:13; Hos 7:16; 8:13; 10:5; Law 25:23
[g]**9:4** Yer 6:20; 16:7; Kum 26:14; Hos 8:13; Hag 2:13-14; Yoe 2:14; Eze 4:13-14
[h]**9:5** Isa 10:3; Yer 5:31; Hos 2:11
[i]**9:6** Isa 5:6; 19:13; Hos 7:11; 8:13; 10:8; Yer 42:22; Isa 32:13; 34:13
[j]6 Memfisi kwa Kiebrania ni Nofu.
[k]**9:7** Mik 7:4; Lk 21:22; Yer 10:15; 16:18; 1Sam 10:11; Mao 2:14; Isa 34:8; 44:25; Ay 31:14; Eze 14:9-10
[l]**9:8** Hos 5:1; Eze 22:26; Yer 6:17; 31:6; Eze 3:17; 35:7
[m]**9:9** Amu 19:16-30; Hos 4:9; 8:13; 10:9; Sef 3:7

Mungu atakumbuka uovu wao
na kuwaadhibu kwa ajili ya
dhambi zao.

10 [a]“Nilipompata Israeli, ilikuwa kama
kupata zabibu jangwani;
nilipowaona baba zenu, ilikuwa
kama kuona
matunda ya kwanza katika mtini.
Lakini walipofika Baal-Peori,
walijiweka wakfu
kwa ile sanamu ya aibu,
nao wakawa najisi
kama kitu kile walichokipenda.
11 [b]Utukufu wa Efraimu utaruka kama
ndege:
hakuna kuzaa, hakuna kuchukua
mimba,
hakuna kutunga mimba.
12 [c]Hata wakilea watoto,
nitamuua kila mmoja.
Ole wao
nitakapowapiga kisogo!
13 [d]Nimemwona Efraimu, kama Tiro,
aliyeoteshwa mahali pazuri.
Lakini Efraimu wataleta
watoto wao kwa mchinjaji.”

14 [e]Wape, Ee Bwana,
je, utawapa nini?
Wape matumbo ya kuharibu mimba
na matiti yaliyokauka.

15 [f]“Kwa sababu ya uovu wao wote
huko Gilgali,
niliwachukia huko.
Kwa sababu ya matendo yao ya
dhambi,
nitawafukuza katika nyumba
yangu.
Sitawapenda tena,
viongozi wao wote ni waasi.
16 [g]Efraimu ameharibiwa,
mzizi wao umenyauka,
hawazai tunda.
Hata kama watazaa watoto,
nitawachinja watoto wao
waliotunzwa vizuri.”

17 [h]Mungu wangu atawakataa
kwa sababu hawakumtii;
watakuwa watu wa kutangatanga
miongoni mwa mataifa.

10 1 [i]Israeli alikuwa mzabibu
uliostawi sana,
alijizalia matunda mwenyewe.
Kadiri matunda yake
yalivyoongezeka,
alijenga madhabahu zaidi;
kadiri nchi yake ilivyostawi,
alipamba mawe yake ya ibada.
2 [j]Moyo wao ni mdanganyifu,
nao sasa lazima wachukue hatia
yao.
Bwana atabomoa madhabahu zao
na kuharibu mawe yao ya ibada.

3 [k]Kisha watasema, “Hatuna mfalme
kwa sababu hatukumheshimu
Bwana.
Lakini hata kama tungelikuwa na
mfalme,
angeweza kutufanyia nini?”
4 [l]Wanaweka ahadi nyingi,
huapa viapo vya uongo
wanapofanya mapatano;
kwa hiyo mashtaka huchipuka
kama magugu ya sumu
katika shamba lililolimwa.

---

[a]**9:10** Hes 25:1-5; Za 106:28-29; Yer 11:13; Hos 4:14; Wim 2:13
[b]**9:11** Hos 4:7; 10:5; Isa 17:3
[c]**9:12** Hos 7:13; Kum 31:17; Eze 24:21
[d]**9:13** Eze 27:3; Za 78:67; Ay 15:22; Mao 2:22
[e]**9:14** Lk 23:29; Hos 9:11; Lk 23:29
[f]**9:15** Hos 4:9, 15; 5:2; 7:2; Isa 1:23; Yer 12:8
[g]**9:16** Hos 5:11; 8:7; Ay 15:32
[h]**9:17** Hos 4:10; 7:13; Kum 28:65; Yer 6:30
[i]**10:1** Eze 15:2; 1Fal 14:23; Hos 4:7; 8:11; 12:11; 13:15
[j]**10:2** 1Fal 18:21; Hos 13:16; Mik 5:13
[k]**10:3** Mik 4:9
[l]**10:4** Hos 4:2; Eze 17:19; Amo 5:7; 6:12; Hos 4:2; Eze 17:19; Amo 5:7; 6:12

5 [a]Watu wanaoishi Samaria huogopa
kwa ajili ya sanamu ya ndama ya
Beth-Aveni.[b]
Watu wake wataiombolezea,
vivyo hivyo kuhani wake wa
kuabudu sanamu,
wale waliokuwa wamefurahia fahari
yake,
kwa sababu itaondolewa kutoka
kwao
kwenda uhamishoni.
6 [c]Itachukuliwa kwenda Ashuru
kama ushuru kwa mfalme mkuu.
Efraimu atafedheheshwa;
Israeli ataaibika kwa ajili ya
sanamu zake za mti.
7 [d]Samaria na mfalme wake wataelea
kama kijiti juu ya uso wa maji.
8 [e]Mahali pa kuabudia sanamu pa
uovu[f] pataharibiwa:
ndiyo dhambi ya Israeli.
Miiba na mibaruti itaota
na kufunika madhabahu zao.
Kisha wataiambia milima,
"Tufunikeni!"
na vilima, "Tuangukieni!"

9 [g]"Tangu siku za Gibea, mmetenda
dhambi, ee Israeli,
huko ndiko mlikobaki.
Je, vita havikuwapata
watenda mabaya huko Gibea?
10 [h]Wakati nitakapopenda,
nitawaadhibu;
mataifa yatakusanywa dhidi yao
ili kuwaweka katika vifungo
kwa ajili ya dhambi zao mbili.
11 [i]Efraimu ni mtamba wa ng'ombe
aliyefundishwa
ambaye hupenda kupura,
hivyo nitamfunga nira
juu ya shingo yake nzuri.
Nitamwendesha Efraimu,
Yuda lazima alime,
naye Yakobo lazima avunjavunje
mabonge ya udongo.
12 [j]Jipandieni wenyewe haki,
vuneni matunda ya upendo usio
na kikomo,
vunjeni ardhi yenu isiyolimwa;
kwa kuwa ni wakati wa kumtafuta
Bwana,
mpaka atakapokuja
na kuwanyeshea juu yenu haki.
13 [k]Lakini mmepanda uovu,
mkavuna ubaya,
mmekula tunda la udanganyifu.
Kwa sababu mmetegemea nguvu
zenu wenyewe
na wingi wa mashujaa wenu,
14 [l]mngurumo wa vita utainuka dhidi
ya watu wako,
ili kwamba ngome zako zote
zitaharibiwa:
kama Shalmani alivyoharibu Beth-
Arbeli katika siku ile ya vita,
wakati mama pamoja na watoto
wao
walipotupwa kwa nguvu ardhini.
15 [m]Ndivyo itakavyotokea kwako, ee
Betheli,
kwa sababu uovu wako ni mkuu.
Siku ile itakapopambazuka,
mfalme wa Israeli ataharibiwa
kabisa.

---

[a]**10:5** Hos 5:8; 8:5-6; 2Fal 23:5; Sef 1:4; Amu 18:17-18; 1Fal 12:28; Kut 32:4; Isa 44:17-20
[b]5 Beth-Aveni maana yake Nyumba ya Ubatili (au Uovu), jina lingine la Betheli kwa dhihaka.
[c]**10:6** 2Fal 16:7; Hos 4:7; 5:13; 11:5; Isa 30:3; Amu 3:15; Yer 48:13
[d]**10:7** Hos 13:11; 10:15
[e]**10:8** 1Fal 12:28-30; Hos 9:6; Kum 9:21; Ufu 6:16; Isa 32:13; Amo 3:14-15; 7:9; Ay 30:6; Eze 6:6; Lk 23:30
[f]8 Yaani *Aveni* kwa Kiebrania, kumaanisha *Beth-Aveni*, jina lingine la Betheli kwa dhihaka.
[g]**10:9** Hos 5:8; Ay 7:11
[h]**10:10** Eze 5:13; Hos 4:9; Amo 8:14
[i]**10:11** Yer 15:12; 31:18
[j]**10:12** Mit 11:18; Yak 3:18; Hos 12:6; Isa 19:22; 45:8; Mhu 11:1; Yer 4:3
[k]**10:13** Ay 4:8; Gal 6:7-8; Za 33:16; Mit 22:8; Hos 7:3; 8:7; 11:12
[l]**10:14** Isa 13:16; 17:3; Mik 5:11; Hos 13:16; 2Fal 17:3
[m]**10:15** Hos 10:7

*Upendo Wa Mungu Kwa Israeli*

11 [a]"Wakati Israeli alipokuwa mtoto,
nilimpenda,
nilimwita mwanangu kutoka
Misri.
2 [b]Lakini kadiri nilivyomwita Israeli,
ndivyo walivyokwenda mbali
nami.
Walitoa dhabihu kwa Mabaali
na kufukiza uvumba kwa vinyago.
3 [c]Mimi ndiye niliyemfundisha
Efraimu kutembea,
nikiwashika mikono;
lakini hawakutambua
kuwa ni mimi niliyewaponya.
4 [d]Niliwaongoza kwa kamba za
huruma ya kibinadamu,
kwa vifungo vya upendo;
niliondoa nira shingoni mwao
nami nikainama kuwalisha.

5 [e]"Je, hawatarudi Misri,
nayo Ashuru haitawatawala
kwa sababu wamekataa kutubu?
6 [f]Panga zitametameta katika miji yao,
zitaharibu makomeo ya malango
yao
na kukomesha mipango yao.
7 [g]Watu wangu wamedhamiria
kuniacha.
Hata kama wakimwita Yeye Aliye
Juu Sana,
kwa vyovyote hatawainua.

8 [h]"Efraimu, ninawezaje kukuacha?
Ee Israeli, ninawezaje kukutoa?
Nitawezaje kukutendea kama Adma?
Nitawezaje kukufanya kama
Seboimu?
Moyo wangu umegeuka ndani
yangu,
huruma zangu zote zimeamshwa.
9 [i]Sitatimiza hasira yangu kali,
wala sitageuka na kumharibu
Efraimu.
Kwa kuwa mimi ndimi Mungu,
wala si mwanadamu,
Aliye Mtakatifu miongoni mwenu.
Sitakuja kwa ghadhabu.
10 [j]Watamfuata Bwana;
atanguruma kama simba.
Wakati angurumapo,
watoto wake watakuja
wakitetemeka
kutoka magharibi.
11 [k]Watakuja wakitetemeka
kama ndege wakitoka Misri,
kama hua wakitoka Ashuru.
Nitawakalisha katika nyumba zao,"
asema Bwana.

*Dhambi Ya Israeli*

12 [l]Efraimu amenizunguka kwa uongo,
nyumba ya Israeli kwa
udanganyifu.
Naye Yuda ni mkaidi dhidi ya
Mungu,
hata kinyume cha yule mwaminifu
Aliye Mtakatifu.

12 1 [m]Efraimu anajilisha upepo;
hufukuzia upepo wa
mashariki kutwa nzima
na kuzidisha uongo na jeuri.
Anafanya mkataba na Ashuru
na kutuma mafuta ya zeituni
Misri.

[a]**11:1** Kut 4:22; Mt 2:15; Yer 2:2; Eze 16:22; Hos 12:9; 13:4
[b]**11:2** Hos 2:13; 4:13; 2Fal 17:15; Isa 65:7; Yer 18:15
[c]**11:3** Kum 1:31; 32:11; Kut 15:26; Yer 30:17
[d]**11:4** Yer 31:2-3, 20; Law 26:13; Kut 16:32; Za 78:25
[e]**11:5** Yer 8:4-6; Hos 7:16; 10:6; Kut 13:17
[f]**11:6** Hos 13:16; Mao 2:9
[g]**11:7** Yer 3:6-7; 8:5; Isa 26:10
[h]**11:8** Mwa 14:8; 19:25; Hos 6:4; Mao 3:32; Yer 7:29; Za 25:6; 1Fal 3:26
[i]**11:9** Kum 13:17
[j]**11:10** Hos 3:5; 6:1-3; Isa 31:4; 42:13; Za 18:45
[k]**11:11** Isa 11:11; Mwa 8:8; Eze 28:26; 34:25-28
[l]**11:12** Hos 4:2; 10:13; Kum 7:9
[m]**12:1** Mwa 41:6; Eze 17:10; 2Fal 17:4; Za 78:67; Hos 4:19; 5:13

2 [a][b]BWANA analo shtaka dhidi ya Yuda,
atamwadhibu Yakobo kwa kadiri ya njia zake
na kumlipa kwa kadiri ya matendo yake.
3 [c]Yakobo akiwa tumboni alishika kisigino cha kaka yake;
kama mwanadamu, alishindana na Mungu.
4 [d]Alishindana na malaika na kumshinda;
alilia na kuomba upendeleo wake.
Alimkuta huko Betheli
na kuzungumza naye huko:
5 [e]BWANA Mungu Mwenye Nguvu Zote,
BWANA ndilo jina lake!
6 [f]Lakini ni lazima urudi kwa Mungu wako;
dumisha upendo na haki,
nawe umngojee Mungu wako siku zote.

7 [g]Mfanyabiashara hutumia vipimo vya udanganyifu;
hupenda kupunja.
8 [h]Efraimu hujisifu akisema,
"Mimi ni tajiri sana; nimetajirika.
Pamoja na utajiri wangu wote hawatakuta ndani yangu
uovu wowote au dhambi."

9 [i]"Mimi ndimi BWANA Mungu wenu
niliyewaleta kutoka Misri;
nitawafanya mkae tena kwenye mahema,
kama vile katika siku
za sikukuu zenu zilizoamriwa.
10 [j]Niliongea na manabii, nikawapa maono mengi
na kusema mifano kupitia wao."

11 [k]Je, Gileadi si mwovu?
Watu wake hawafai kitu!
Je, hawatoi dhabihu za mafahali huko Gilgali?
Madhabahu zao zitakuwa
kama malundo ya mawe
katika shamba lililolimwa.
12 [l]Yakobo alikimbilia katika nchi ya Aramu;
Israeli alitumika ili apate mke,
ili aweze kulipa kwa ajili yake alichunga kondoo.
13 [m]BWANA alimtumia nabii
kumpandisha Israeli kutoka Misri,
kwa njia ya nabii alimtunza.
14 [n]Lakini Efraimu amemchochea sana hasira;
Bwana wake ataleta juu yake
hatia yake ya kumwaga damu naye atamlipiza
kwa ajili ya dharau yake.

### *Hasira Ya Bwana Dhidi Ya Israeli*

13 [o]Wakati Efraimu alipozungumza, watu walitetemeka,
alikuwa ametukuzwa katika Israeli.
Lakini alikuwa na hatia ya kumwabudu Baali
naye akafa.
2 [p]Sasa wanatenda dhambi zaidi na zaidi;
wanajitengenezea sanamu
kutokana na fedha yao,
vinyago vilivyotengenezwa kwa uhodari,
vyote kazi ya fundi stadi.

---

[a]**12:2** Ay 10:2
[b]**12:2** Mik 6:2; Hos 4:9; 9:15; Kut 32:34; Amo 2:4
[c]**12:3** Mwa 25:26; 32:24-29
[d]**12:4** Mwa 12:8; 28:12-15; 35:15
[e]**12:5** Kut 3:15
[f]**12:6** Mik 6:8; 7:7; Za 106:13; Eze 18:30; Isa 19:22; Yoe 2:12; Yer 22:3
[g]**12:7** Law 19:26; Amo 8:5
[h]**12:8** Za 62:10; Ufu 3:17; Eze 28:5
[i]**12:9** Law 23:43; Hos 2:15; Neh 8:17
[j]**12:10** Amu 14:12; Eze 20:49; 2Fal 17:13; Yer 7:25
[k]**12:11** Amo 4:4; Hos 4:15; 6:8; 8:11
[l]**12:12** Mwa 28:5; 29:18
[m]**12:13** Kut 14:19-22; Isa 63:11-14; Kut 13:3; Hos 11:1
[n]**12:14** Eze 18:13; Dan 11:18
[o]**13:1** Mit 18:12; Amu 8:1; 12:1; Hos 11:2
[p]**13:2** Isa 46:6; Yer 10:4; 44:8; Isa 44:17-20; Hos 8:4; 1Fal 19:18

Inasemekana kuhusu hawa watu,
"Hutoa dhabihu za binadamu
na kubusu sanamu za ndama."
3 [a][b]Kwa hiyo watakuwa kama ukungu wa asubuhi,
kama umande wa alfajiri utowekao,
kama makapi yapeperushwayo
kutoka sakafu ya kupuria nafaka,
kama moshi utorokao kupitia dirishani.

4 [c]"Bali mimi ndimi BWANA Mungu wenu,
niliyewaleta ninyi toka Misri.
Msimkubali Mungu mwingine ila mimi,
hakuna Mwokozi isipokuwa mimi.
5 [d]Niliwatunza huko jangwani,
katika nchi yenye joto liunguzalo.
6 [e]Nilipowalisha, walishiba,
waliposhiba, wakajivuna,
kisha wakanisahau mimi.
7 [f]Kwa hiyo nitakuja juu yao kama simba,
kama chui nitawavizia kando ya njia.
8 [g]Kama dubu aliyenyang'anywa watoto wake,
nitawashambulia na kurarua vifua vyenu.
Kama simba nitawala;
mnyama pori atawararua vipande vipande.

9 [h]"Ee Israeli, umeangamizwa,
kwa sababu wewe u kinyume nami,
kinyume na msaidizi wako.
10 [i]Yuko wapi mfalme wako,
ili apate kukuokoa?
Wako wapi watawala wako katika miji yako yote
ambao ulisema kuwahusu,
'Nipe mfalme na wakuu'?
11 [j]Hivyo katika hasira yangu nilikupa mfalme
na katika ghadhabu yangu nilimwondoa.
12 [k]Kosa la Efraimu limehifadhiwa,
dhambi zake zimewekwa katika kumbukumbu.
13 [l]Utungu kama wa mwanamke anayejifungua mtoto humjia,
lakini yeye ni mtoto asiyekuwa na hekima;
wakati utakapowadia hatatoka
katika tumbo la mama yake.

14 [m]"Nitawakomboa watu hawa kutoka nguvu za kaburi,
nitawakomboa kutoka mautini.
Yako wapi, ee mauti, mateso yako?
Uko wapi, ee kuzimu, uharibifu wako?

"Sitakuwa na huruma,
15 [n]hata ingawa Efraimu atastawi
miongoni mwa ndugu zake.
Upepo wa mashariki kutoka kwa BWANA utakuja,
ukivuma kutoka jangwani,
chemchemi yake haitatoa maji
na kisima chake kitakauka.
Ghala lake litatekwa
hazina zake zote.

---

[a]**13:3** Hos 6:4; Ay 13:25; Dan 2:35; Za 68:2
[b]**13:3** Isa 17:13
[c]**13:4** Yer 2:6; Isa 43:10; 45:21-22; Hos 2:20; 12:9; Kut 20:3; Za 18:46
[d]**13:5** Kum 1:19; 2:7; 32:10; 8:15; 32:10
[e]**13:6** Mit 30:7-9; Yer 7:5; Eze 28:5; Kum 32:18; Isa 17:10; Hos 2:13; 4:7
[f]**13:7** Ay 10:16; Yer 4:7; Mao 3:10
[g]**13:8** 2Sam 17:8; Za 17:12; 50:22; Mao 3:10; Hos 2:12
[h]**13:9** Yer 2:17-19; Kum 33:29
[i]**13:10** 2Fal 17:4; 1Sam 8:6; Hos 7:7; 8:4
[j]**13:11** Yos 24:20; 1Sam 13:14; Hes 11:20; 1Fal 14:10; Hos 10:7
[k]**13:12** Kum 32:34; Ay 14:7
[l]**13:13** Isa 13:8; Mik 4:9-10; Isa 66:9; 2Fal 19:3
[m]**13:14** 1The 4:14-17; Za 16:10; 49:15; Eze 37:12-13; 1Kor 15:54-55; Ufu 21:4
[n]**13:15** Ay 1:19; Eze 19:12; Yer 20:5; 51:36; Hos 4:19

16 [a]Watu wa Samaria ni lazima wabebe
hatia yao,
kwa sababu wameasi dhidi ya
Mungu wao.
Wataanguka kwa upanga;
watoto wao wadogo watatupwa
kwa nguvu ardhini,
wanawake wao walio na mimba
watatumbuliwa."

*Toba Iletayo Baraka*

14 [b]Rudi, ee Israeli, kwa BWANA
Mungu wako.
Dhambi zako zimekuwa
ndilo anguko lako!
2 [c]Chukueni maneno pamoja nanyi,
mkamrudie BWANA.
Mwambieni:
"Samehe dhambi zetu zote
na utupokee kwa neema,
ili tuweze kutoa matunda yetu
kama sadaka za mafahali.
3 [d]Ashuru hawezi kutuokoa,
hatutapanda farasi wa vita.
Kamwe hatutasema tena 'Miungu
yetu'
kwa kile ambacho mikono yetu
wenyewe imetengeneza,
kwa kuwa kwako wewe yatima
hupata huruma."

4 [e]"Nitaponya ukaidi wao
na kuwapenda kwa hiari yangu,
kwa kuwa hasira yangu
imeondoka kwao.
5 [f]Nitakuwa kama umande kwa Israeli;
atachanua kama yungiyungi.
Kama mwerezi wa Lebanoni
atashusha mizizi yake chini;
6 [g]matawi yake yatatanda.
Fahari yake itakuwa kama mti wa
mzeituni,
harufu yake nzuri kama mwerezi
wa Lebanoni.
7 [h]Watu wataishi tena kwenye kivuli
chake.
Atastawi kama nafaka.
Atachanua kama mzabibu,
nao umaarufu wake utakuwa
kama divai itokayo Lebanoni.
8 [i]Ee Efraimu, nina shughuli gani tena
na sanamu?
Nitamjibu na kumtunza.
Mimi ni kama msunobari wenye
majani mabichi;
kuzaa kwako matunda kunatoka
kwangu."

9 [j]Ni nani mwenye hekima?
Atayatambua mambo haya.
Ni nani mwenye ufahamu? Huyu
atayaelewa.
Njia za BWANA ni adili;
wenye haki huenda katika njia
hizo,
lakini waasi watajikwaa ndani
yake.

---

[a]**13:16** 2Fal 8:12; 15:16; 17:5; Hos 7:14; 10:2, 14; Isa 13:16; Amo 1:13
[b]**14:1** Hos 5:5; 9:7; 12:6; Yer 3:12; Isa 19:22
[c]**14:2** Rum 8:26; Za 51:16-17; Mik 7:18-19; Ebr 13:15; Kut 34:9
[d]**14:3** Mik 5:10; Isa 31:1; Hos 5:13; 8:6; Yer 49:11; Za 10:14; 33:17
[e]**14:4** Isa 30:26; 55:1; Hos 6:1; Yer 2:19; 31:20; Sef 3:17; Ay 13:16
[f]**14:5** Wim 2:1; Isa 18:4; 35:2; Ay 29:19; Mwa 27:28
[g]**14:6** Za 52:8; 92:12; Yer 11:16; Wim 4:11
[h]**14:7** Za 91:1-4; Hos 2:22; Eze 17:23; Mwa 40:10
[i]**14:8** Yer 31:18; Yak 1:17; Isa 37:24
[j]**14:9** Za 107:43; Mit 10:29; Dan 12:10; Sef 3:5; Mdo 13:10; Isa 1:28; 26:7

# YOELI

1 [a]Neno la BWANA ambalo lilimjia Yoeli mwana wa Pethueli.

*Uvamizi Wa Nzige*

2 [b]Sikilizeni hili, enyi wazee;
sikilizeni, ninyi nyote mnaoishi katika nchi.
Je, jambo kama hili lilishawahi kutokea
katika siku zenu au katika siku za babu zenu?
3 [c]Waelezeni watoto wenu,
na watoto wenu wawaambie watoto wao,
na watoto wao kwa kizazi kitakachofuata.
4 [d]Kilichosazwa na kundi la tunutu
nzige wakubwa wamekula,
kilichosazwa na nzige wakubwa
parare wamekula,
kilichosazwa na parare
madumadu wamekula.
5 [e]Amkeni, enyi walevi, mlie!
Pigeni yowe enyi wanywaji wote wa mvinyo,
pigeni yowe kwa sababu ya mvinyo mpya,
kwa kuwa mmenyang'anywa
kutoka midomoni mwenu.
6 [f]Taifa limevamia nchi yangu,
lenye nguvu tena lisilo na idadi;
lina meno ya simba,
magego ya simba jike.
7 [g]Limeharibu mizabibu yangu
na kuangamiza mitini yangu.
Limebambua magome yake
na kuyatupilia mbali,
likayaacha matawi yake yakiwa meupe.

8 [h]Omboleza kama bikira aliyevaa nguo ya gunia
anayehuzunika kwa ajili ya mume wa ujana wake.
9 [i]Sadaka za nafaka na sadaka za kinywaji
zimekatiliwa mbali kutoka nyumba ya BWANA.
Makuhani wanaomboleza,
wale wanaohudumu mbele za BWANA.
10 [j]Mashamba yameharibiwa,
ardhi imekauka;
nafaka imeharibiwa,
mvinyo mpya umekauka,
mafuta yamekoma.
11 [k]Kateni tamaa, enyi wakulima,
lieni, enyi mlimao mizabibu;
huzunikeni kwa ajili ya ngano na shayiri,
kwa sababu mavuno ya shambani yameharibiwa.
12 [l]Mzabibu umekauka
na mtini umenyauka;
mkomamanga, mtende na mtofaa,
miti yote shambani, imekauka.
Hakika furaha yote ya mwanadamu
imeondoka.

---

[a]**1:1** 2Pet 1:21; Ebr 1:1; Yer 1:2; Mdo 2:16
[b]**1:2** Yoe 2:2, 16; Hos 4:1; 5:1; Isa 7:17; Kum 4:32; Dan 12:1; Mt 24:21
[c]**1:3** Kut 10:2; Za 78:4
[d]**1:4** Kut 10:4, 14-15; Amo 7:1; Neh 3:15; Kum 28:39
[e]**1:5** Isa 24:7; 32:10; Yoe 3:3
[f]**1:6** Yoe 2:2, 11, 25; Ufu 9:8; Mit 30:25; Za 105:35
[g]**1:7** Isa 5:8; Amo 4:9
[h]**1:8** Isa 22:2; Amo 8:10; Mit 2:17
[i]**1:9** Yoe 2:14; Hos 9:4; Isa 22:12
[j]**1:10** Isa 5:6; 24:4; Yer 3:3; Hos 9:2; Hes 18:12; Yer 12:11
[k]**1:11** Yer 14:3; Ay 6:20; Amo 5:16; Kut 9:31; Isa 17:11
[l]**1:12** Isa 15:6; Kut 28:33; Isa 16:8; Hos 9:1-2; Hag 2:19; Yer 48:33

*Wito Wa Toba*

13 [a]Vaeni nguo ya gunia, enyi
makuhani, muomboleze;
pigeni yowe, enyi mnaohudumu
madhabahuni.
Njooni, vaeni nguo ya gunia usiku
kucha,
enyi mnaohudumu mbele za
Mungu wangu;
kwa kuwa sadaka za nafaka na
sadaka za kinywaji
zimezuiliwa kufika katika nyumba
ya Mungu wenu.
14 [b]Tangazeni saumu takatifu;
liiteni kusanyiko takatifu.
Iteni wazee
na wote waishio katika nchi
waende katika nyumba ya BWANA
Mungu wenu,
wakamlilie BWANA.

15 [c]Ole kwa siku hiyo!
Kwa kuwa siku ya BWANA iko
karibu;
itakuja kama uharibifu
kutoka kwa Mwenyezi.[d]

16 Je, chakula hakikukatiliwa mbali
mbele ya macho yetu:
furaha na shangwe
kutoka nyumba ya Mungu wetu?
17 Mbegu zinakauka
chini ya mabonge ya udongo.
Ghala zimeachwa katika uharibifu,
ghala za nafaka zimebomolewa,
kwa maana hakuna nafaka.
18 Jinsi gani ng'ombe wanavyolia!
Makundi ya mifugo yanahangaika
kwa sababu hawana malisho;
hata makundi ya kondoo
yanateseka.

19 Kwako, Ee BWANA, naita,
kwa kuwa moto umeteketeza
malisho ya mbugani
na miali ya moto imeunguza
miti yote shambani.
20 Hata wanyama wa porini
wanakuonea shauku;
vijito vya maji vimekauka,
na moto umeteketeza
malisho yote ya mbugani.

*Jeshi La Nzige*

2 [d]Pigeni tarumbeta katika Sayuni;
pigeni mbiu katika mlima
wangu mtakatifu.
Wote waishio katika nchi na
watetemeke,
kwa kuwa siku ya BWANA inakuja.
Iko karibu,
2 [f]siku ya giza na huzuni,
siku ya mawingu na utusitusi.
Kama mapambazuko yasambaavyo
toka upande huu wa milima
hata upande mwingine
jeshi kubwa na lenye nguvu
linakuja.
Jambo kama hili halijakuwepo tangu
zamani
wala halitakuwepo tena kamwe
kwa vizazi vijavyo.
3 [g]Mbele yao moto unateketeza,
nyuma yao miali ya moto
inawaka kwa nguvu.
Mbele yao nchi iko kama bustani ya
Edeni,
nyuma yao ni jangwa lisilofaa:
hakuna kitu kinachowaepuka.
4 Wanaonekana kama farasi;
wanakwenda mbio
kama askari wapanda farasi.
5 [h]Wanatoa sauti kama magari ya vita,
wanaporukaruka juu ya vilele vya
milima,

[a]**1:13** Mwa 37:34; Yer 4:8; 2:17; Hos 9:4; Yoe 2:14
[b]**1:14** 2Nya 20:3-4; Yon 3:8; Hos 4:1
[c]**1:15** Yer 30:7; 46:10; Isa 2:12; Eze 30:3; Amo 5:8
[d]15 Mwenyezi hapa ina maana ya Shaddai kwa Kiebrania.
[d]**2:1** Hos 10:2, 7; Kut 15:17; Oba 1:15; Sef 1:14-16; Eze 12:23
[f]**2:2** Ay 9:7; Isa 8:22; 13:10; Amo 5:18; Kut 10:14; Dan 9:12; Mt 24:21; Eze 34:12
[g]**2:3** Za 97:3; 105:34-35; Kut 10:12-15; Isa 14:17; Zek 7:14; Isa 1:31
[h]**2:5** Ufu 9:9; Isa 5:24; 30:30

kama mlio wa miali ya moto ilayo
mabua,
kama jeshi kubwa lililojipanga
kwa ajili ya vita.

6 [a]Wanapoonekana, mataifa yanakuwa
katika maumivu makuu;
kila uso unabadilika rangi.
7 [b]Wanashambulia kama wapiganaji
wa vita;
wanapanda kuta kama askari.
Wote wanatembea katika safu,
hawapotoshi safu zao.
8 Hakuna anayemsukuma mwenzake;
kila mmoja anakwenda mbele
moja kwa moja.
Wanapita katika vizuizi
bila kuharibu safu zao.
9 [c]Wanaenda kasi kuingia mjini;
wanakimbia ukutani.
Wanaingia ndani ya nyumba;
kwa kuingilia madirishani kama
wevi.

10 [d]Mbele yao dunia inatikisika,
anga linatetemeka,
jua na mwezi vinatiwa giza,
na nyota hazitoi mwanga wake
tena.
11 [e]BWANA anatoa mshindo wa
ngurumo
mbele ya jeshi lake;
majeshi yake hayana idadi,
ni wenye nguvu nyingi
wale ambao hutii agizo lake.
Siku ya BWANA ni kuu,
ni ya kutisha.
Ni nani anayeweza kuistahimili?

*Rarueni Mioyo Yenu*

12 [f]"Hata sasa," asema BWANA,
"nirudieni kwa mioyo yenu yote,
kwa kufunga, kwa kulia na
kuomboleza."

13 [g]Rarueni mioyo yenu
na siyo mavazi yenu.
Mrudieni BWANA, Mungu wenu,
kwa maana yeye ndiye mwenye
neema
na mwingi wa huruma,
si mwepesi wa hasira, ni mwingi wa
upendo,
huona huruma, hujizuia kuleta
maafa.
14 [h]Ni nani ajuaye? Yeye aweza
kugeuka na kuwa na huruma
na kuacha baraka nyuma yake:
sadaka za nafaka na sadaka za
vinywaji
kwa ajili ya BWANA Mungu wenu.

15 [i]Pigeni tarumbeta katika Sayuni,
tangazeni saumu takatifu,
liiteni kusanyiko takatifu.
16 [j]Wakusanyeni watu,
wekeni wakfu kusanyiko;
waleteni pamoja wazee,
wakusanyeni watoto,
wale wanyonyao maziwa.
Bwana arusi na atoke chumbani
mwake
na bibi arusi naye atoke katika
chumba chake.
17 [k]Makuhani, ambao wanahudumu
mbele za BWANA,
na walie katikati ya ukumbi
wa Hekalu na madhabahu.

---

[a]**2:6** Yer 8:21; Isa 13
[b]**2:7** Isa 5:27; Mit 30:27; Ay 16:14
[c]**2:9** Yer 9:21; Kut 10:6
[d]**2:10** Isa 5:30; 13:10; Za 18:7; 102:26; Ufu 9:2; Ay 9:7; Eze 38:19
[e]**2:11** Isa 2:12; Hes 24:23; Ufu 6:17; 18:8; Sef 2:11; Eze 30:3; Yoe 1:15; Yer 50:34; Mal 3:2; Za 29:3
[f]**2:12** Kum 4:30; Hos 12:6; Eze 33:11; 1Sam 7:3
[g]**2:13** Za 34:18; 51:17; 86:5; Mwa 37:29; Hes 14:6; Kut 34:6; Yon 4:2; Isa 57:15; 2Fal 22:19; Mt 5:3-4; Ay 1:20
[h]**2:14** Yer 26:3; 31:14; Yn 3:9; Sef 2:3; Isa 65:8; Zek 8:13; Yos 14:12; Amo 5:15; Hag 2:19; Mal 3:10
[i]**2:15** 2Nya 20:3; Hes 10:2-3; Yer 36:9
[j]**2:16** Kut 19:10; 2Nya 20:13; 1Kor 7:5; Za 19
[k]**2:17** Eze 8:16; Mt 23:35; Kum 9:26-29; Ay 17:6; Za 42:3; Kut 32:11; Isa 37:20; Yoe 1:13; Isa 22:12

Waseme, "Wahurumie watu wako,
Ee BWANA.
Usifanye urithi wako kitu cha
kudharauliwa,
neno la dhihaka kati ya mataifa.
Kwa nini wasemezane miongoni
mwao,
'Yuko wapi Mungu wao?' "

*Jibu La BWANA*

18 [a]Kisha BWANA atakuwa na wivu kwa
ajili ya nchi yake
na kuwa na huruma juu ya watu
wake.
19 [b]BWANA atawajibu:
"Ninawapelekea nafaka,
mvinyo mpya na mafuta,
vya kuwatosha ninyi
hadi mridhike kabisa;
kamwe sitawafanya tena
kitu cha kudharauliwa na mataifa.

20 [c]"Nitafukuza jeshi la kaskazini likae
mbali nanyi,
nikilisukuma ndani ya jangwa,
askari wa safu za mbele wakienda
ndani ya bahari ya mashariki
na wale wa safu za nyuma
katika bahari ya magharibi.
Uvundo wake utapaa juu;
harufu yake itapanda juu."

Hakika ametenda mambo makubwa.
21 [d]Usiogope, ee nchi;
furahi na kushangilia.
Hakika BWANA ametenda mambo
makubwa.
22 [e]Msiogope, enyi wanyama pori,
kwa kuwa mbuga za malisho yenu
zinarudia ubichi.
Miti nayo inazaa matunda,
mtini na mzabibu inatoa utajiri
wake.
23 [f]Furahini, enyi watu wa Sayuni,
shangilieni katika BWANA Mungu
wenu,
kwa kuwa amewapa mvua za vuli
kwa kipimo cha haki.
Anawapelekea mvua nyingi,
mvua ya vuli na ya masika, kama
mwanzoni.
24 [g]Sakafu za kupuria zitajaa nafaka,
mapipa yatafurika mvinyo mpya
na mafuta.

25 [h]"Nitawalipa kwa ajili ya miaka ile
iliyoliwa na nzige:
parare, madumadu na tunutu,
jeshi langu kubwa ambalo
nililituma katikati yenu.
26 [i]Mtakuwa na wingi wa vyakula
mpaka mshibe,
na mtalisifu jina la BWANA Mungu
wenu,
ambaye amefanya maajabu kwa ajili
yenu;
kamwe watu wangu
hawataaibishwa tena.
27 [j]Ndipo mtakapojua kwamba mimi
niko katika Israeli
kwamba mimi ndimi BWANA
Mungu wenu,
na kwamba hakuna mwingine;
kamwe watu wangu hawataaibika
tena.

*Siku Ya BWANA*

28 [k]"Hata itakuwa, baada ya hayo,
nitamimina Roho wangu juu ya
wote wenye mwili.

---

[a]**2:18** Isa 26:11; 42:13; Zek 8:2; 1:14; Kum 32:36; Za 103:13; 72:13
[b]**2:19** Yer 31:12; Eze 34:29; Za 4:7; Law 26:5
[c]**2:20** Yer 1:14-15; Zek 14:8; Kum 11:24; Kut 10:19; Isa 34:3
[d]**2:21** Sef 3:16-17; Isa 25:1; 29:22; 54:4; 1Yn 4:18
[e]**2:22** Yoe 1:18-20; Zek 8:12; Za 65:12; Hes 16:14; 1Fal 4:25
[f]**2:23** Hab 3:18; Yak 5:7; Za 28:7; 33:21; Law 26:4
[g]**2:24** Law 26:10; Mal 3:10; Mit 3:10; Amo 9:13; Yoe 3:18
[h]**2:25** Kut 14:10; Amo 4:9
[i]**2:26** Law 23:40; 26:5; Isa 25:1; 29:22; 62:9; Za 126:3; Mik 6:14
[j]**2:27** Kut 6:2; Isa 44:8; 45:5; 54:4; Yoe 3:17; Law 26:11; Sef 3:11
[k]**2:28** Yn 7:38; 11:2; Eze 39:29; Mdo 21:9; Hes 11:17; Gal 3:14; 1Sam 19:20

Wana wenu na binti zenu watatabiri,
wazee wenu wataota ndoto,
na vijana wenu wataona maono.
29 [a]Hata juu ya watumishi wangu,
wanaume kwa wanawake,
katika siku zile nitamimina Roho
wangu.
30 [b]Nami nitaonyesha maajabu katika
mbingu
na duniani:
damu, moto na mawimbi ya
moshi.
31 [c]Jua litageuzwa kuwa giza
na mwezi kuwa mwekundu kama
damu,
kabla ya kuja siku ya BWANA
ile kuu na ya kutisha.
32 [d]Na kila mtu atakayeliitia
jina la BWANA ataokolewa.
Kwa maana juu ya Mlima Sayuni na
katika Yerusalemu
kutakuwepo wokovu,
kama BWANA alivyosema,
miongoni mwa walionusurika
ambao BWANA awaita.

*Mataifa Yahukumiwa*

3 [e]"Katika siku hizo na wakati huo,
nitakaporejesha neema ya
Yuda na Yerusalemu,
2 [f]nitayakusanya mataifa yote na
kuyaleta
katika Bonde la Yehoshafati[g]
Hapo nitaingia kwenye hukumu
dhidi yao
kuhusu urithi wangu, watu wangu
Israeli,
kwa kuwa waliwatawanya watu
wangu
miongoni mwa mataifa
na kuigawa nchi yangu.
3 [h]Wanawapigia kura watu wangu
na kuwauza wavulana ili kupata
makahaba;
waliwauza wasichana
ili wapate kunywa mvinyo.

4 [i]"Sasa una nini dhidi yangu, ee Tiro
na Sidoni, nanyi nchi zote za Ufilisti?
Je, mnanilipiza kwa yale niliyoyafanya?
Kama mnalipa, mimi nitalipiza juu ya
vichwa vyenu kwa kasi na kwa haraka
yale mliyoyatenda. 5 [j]Kwa kuwa mlichukua
fedha na dhahabu yangu pia mkabeba
hazina zangu nzuri sana mkapeleka kwenye
mahekalu yenu. 6 [k]Mliwauza watu wa Yuda
na Yerusalemu kwa Wayunani, ili kwamba
mpate kuwapeleka mbali na nchi yao.
7 [l]"Tazama nitawaamsha kutoka zile
sehemu mlizowauza, nami nitawalipiza
juu ya vichwa vyenu kile mlichofanya.
8 [m]Nitawauza wana wenu na binti zenu kwa
watu wa Yuda, nao watawauza kwa Waseba,
taifa lililo mbali." BWANA amesema.

9 [n]Tangazeni hili miongoni mwa
mataifa:
Jiandaeni kwa vita!
Amsha askari!
Wanaume wote wapiganaji
wasogee karibu na kushambulia.
10 [o]Majembe yenu yafueni yawe panga
na miundu yenu ya kukatia iwe
mikuki.
Aliye dhaifu na aseme,
"Mimi nina nguvu!"

[a]**2:29** 1Kor 12:13; Gal 3:28; Eze 36:27
[b]**2:30** Lk 21:11; Mk 13:24-25
[c]**2:31** Isa 22:5; Mt 24:29; Isa 13:9-10; Mal 3:2; Yer 4:23; Yoe 1:15
[d]**2:32** Rum 9:27; 10:13; Oba 1:17; Mik 4:7; 7:18; Isa 11:11; 46:13; Za 106:8; 50:12; Yer 33:3; Mwa 4:26; Mdo 2:21, 39
[e]**3:1** Kum 30:3; Yer 16:15; 40:5; Eze 3:20; 38:8
[f]**3:2** Zek 14:2; Isa 13:9; 2Nya 20:26; Isa 66:16; Yer 2:35; Sef 3:8; Mwa 11:4; Law 26:33
[g]2 Yehoshafati maana yake BWANA huhukumu.
[h]**3:3** Oba 1:11; Amo 2:6; Ay 6:27; Eze 24:6
[i]**3:4** Mwa 10:15; Mt 11:21; Yak 2:13; Lk 18:7; Amo 1:6-9; Isa 14:29-31; 34:8; Za 87:4; Eze 25:15-17
[j]**3:5** 1Fal 15:18; 2Nya 21:16-17
[k]**3:6** Eze 27:13; Zek 9:13
[l]**3:7** Isa 43:5-6; 66:6; Yer 23:8
[m]**3:8** Eze 23:42; Isa 14:2; 60:14; Mwa 10:7; Yer 30:16; 2Nya 9:1
[n]**3:9** Isa 8:9; Yer 46:4
[o]**3:10** Zek 12:8; Isa 2:4; Mik 4:3; Hes 25:7

11 [a]Njooni haraka, ninyi mataifa yote
kutoka pande zote,
kusanyikeni huko.

Shusha wapiganaji wako, Ee
BWANA!

12 [b]"Mataifa na yaamshwe;
na yasonge mbele kuelekea Bonde
la Yehoshafati,
kwa kuwa nitaketi mahali pale
kuhukumu mataifa yote yaliyoko
kila upande.
13 [c]Tia mundu,
kwa kuwa mavuno yamekomaa.
Njooni, mkanyage zabibu,
kwa kuwa shinikizo la kukamua
zabibu limejaa
na mapipa yanafurika:
kwa kuwa uovu wao ni mkubwa!"

14 [d]Umati mkubwa, umati mkubwa
katika bonde la uamuzi!
Kwa kuwa siku ya BWANA ni karibu
katika bonde la uamuzi.
15 Jua na mwezi vitatiwa giza,
na nyota hazitatoa mwanga wake
tena.
16 [e]BWANA atanguruma kutoka Sayuni
na mshindo wa ngurumo kutoka
Yerusalemu;
dunia na mbingu vitatikisika.
Lakini BWANA atakuwa kimbilio la
watu wake,
ngome imara kwa ajili ya watu wa
Israeli.

*Baraka Kwa Watu Wa Mungu*

17 [f]"Ndipo mtakapojua kwamba Mimi,
BWANA Mungu wenu,
nakaa Sayuni, mlima wangu
mtakatifu.
Yerusalemu utakuwa mtakatifu;
kamwe wageni hawatavamia tena.

18 [g]"Katika siku hiyo milima
itadondosha divai mpya,
na vilima vitatiririka maziwa;
mabonde yote ya Yuda yatatiririka
maji.
Chemchemi itatiririka kutoka
kwenye nyumba ya BWANA
na kunywesha Bonde la Shitimu.[h]
19 [i]Lakini Misri itakuwa ukiwa,
Edomu itakuwa jangwa tupu,
kwa sababu ya jeuri waliofanya kwa
watu wa Yuda,
ambao katika nchi yao
walimwaga damu isiyo na hatia.
20 [j]Yuda itakaliwa na watu milele
na Yerusalemu itadumu vizazi
vyote.
21 [k]Hatia yao ya damu, ambayo
sijasamehe,
nitasamehe."

BWANA anakaa Sayuni!

---

[a]**3:11** Eze 38:15-16; Sef 3:8; Isa 13:3
[b]**3:12** Za 96:13; 82:1; 2Nya 20:26; Isa 2:4
[c]**3:13** Isa 17:5; Ufu 14:15-20; Amu 6:11; Mt 13:39; Mk 4:29; Yer 51:33; Hos 6:11
[d]**3:14** Isa 2:4; 13:4; 34:2-8; Sef 1:7; Yoe 1:15; Eze 36:5
[e]**3:16** Amu 5:4; Isa 14:16; 25:4; 42:13; 2Sam 22:3; Zek 9:12; Eze 38:19
[f]**3:17** Yoe 2:27; Za 74:2; Isa 4:3; 35:8; Ufu 21:27; Nah 1:15; Kut 6:7; Yer 31:40; Eze 44:9
[g]**3:18** Kut 3:8; Eze 47:1; Zek 13:1; Wim 5:1; Isa 25:6; 30:25; 35:6; 44:3; Ufu 22:1-2; Hes 25:1; Yoe 2:24
[h]18 Au: *Bonde la Migunga.*
[i]**3:19** Yer 51:35; Oba 1:10; Isa 11:14; 34:11
[j]**3:20** Ezr 9:12; Amo 9:15
[k]**3:21** Eze 36:25; 48:35; Isa 1:15; 59:20; Za 74:2; Zek 8:3

# AMOSI

1 [a]Maneno ya Amosi, mmoja wa wachunga wanyama wa Tekoa: yale aliyoyaona kuhusu Israeli miaka miwili kabla ya tetemeko la ardhi, wakati Uzia alikuwa mfalme wa Yuda, na Yeroboamu mwana wa Yehoashi alikuwa mfalme wa Israeli.

2 [b]Alisema:

"BWANA ananguruma toka Sayuni,
pia ananguruma kutoka Yerusalemu;
malisho ya wachunga wanyama yanakauka,
kilele cha Karmeli kinanyauka."

*Hukumu Juu Ya Majirani Wa Israeli*

3 [c]Hili ndilo asemalo BWANA:

"Kwa dhambi tatu za Dameski,
hata kwa dhambi nne, sitaizuia ghadhabu yangu.
Kwa sababu aliipura Gileadi
kwa vyombo vya chuma vyenye meno.
4 [d]Nitatuma moto juu ya nyumba ya Hazaeli
ambao utateketeza ngome za Ben-Hadadi.
5 [e]Nitalivunja lango la Dameski;
nitamwangamiza mfalme aliyeko katika Bonde la Aveni,[f]
na yeye ambaye anaishika fimbo ya utawala katika Beth-Edeni.
Watu wote wa Aramu watakwenda uhamishoni huko Kiri,"
asema BWANA.

6 [g]Hili ndilo asemalo BWANA:

"Kwa dhambi tatu za Gaza,
hata kwa dhambi nne, sitaizuia ghadhabu yangu.
Kwa sababu walichukua mateka jumuiya nzima
na kuwauza kwa Edomu,
7 [h]nitatuma moto juu ya kuta za Gaza
ambao utateketeza ngome zake.
8 [i]Nitamwangamiza mfalme wa Ashdodi
na yeye aishikaye fimbo ya utawala katika Ashkeloni.
Nitaugeuza mkono wangu dhidi ya Ekroni,
hadi Mfilisti wa mwisho atakapokufa,"
asema BWANA Mwenyezi.

9 [j]Hili ndilo asemalo BWANA:

"Kwa dhambi tatu za Tiro,
hata kwa dhambi nne, sitaizuia ghadhabu yangu.
Kwa sababu ameuza jumuiya nzima ya mateka kwa Edomu,
na kutokujali mapatano ya undugu,
10 [k]Nitatuma moto kwenye kuta za Tiro
ambao utateketeza ngome zake."

11 [l]Hili ndilo BWANA asemalo:

"Kwa dhambi tatu za Edomu,
hata kwa dhambi nne, sitaizuia ghadhabu yangu.

---

[a]**1:1** 2Sam 14:2; Zek 14:5; 2Fal 14:21-23; Hos 1:1; 2Nya 11:6; Za 78:70; 2Nya 26:23
[b]**1:2** Isa 42:13; Yoe 3:16; Amo 9:3; Yer 12:4; Za 29:3
[c]**1:3** Isa 8:4; 7:9; 17:1-3; 8:4; 2Fal 10:33; Amo 2:6
[d]**1:4** Eze 30:8; Yer 17:27; 49:23-27; 1Fal 20:1; 19:17; 2Fal 6:24
[e]**1:5** Yer 51:30; 49:27; Isa 7:1, 16; 22:6; Zek 9:1; 2Fal 16:9
[f]5 Bonde la Aveni maana yake Bonde la Uovu.
[g]**1:6** 2Nya 28:18; 1Sam 6:17; Mwa 10:19; 14:6; Oba 1:11; Sef 2:4
[h]**1:7** 2Fal 18:8
[i]**1:8** 2Nya 26:6; Za 81:14; Eze 25:16; Isa 14:28-32; 34:8; Sef 2:4-7
[j]**1:9** Isa 23:1-18; 1Fal 5:12; 9:11-14; Yer 25:22; Yoe 3:4
[k]**1:10** Yer 47:6; Eze 26:2-4; Isa 23:1-18; 34:8; Zek 9:1-4
[l]**1:11** Yer 49:7-22; Eze 25:12-14; Zek 1:15; Mal 1:4; Za 83:6; Hes 20:14-21; 2Nya 28:17

Kwa sababu alimfuatia ndugu yake
kwa upanga,
alikataa kuonyesha huruma
yoyote,
kwa sababu hasira yake kali
iliendelea kupanda wakati
wote
na ghadhabu iliwaka bila
kuzuiliwa.
12 [a]Nitatuma moto juu ya Temani
ambao utateketeza ngome za
Bosra."

13 [b]Hili ndilo asemalo BWANA:

"Kwa dhambi tatu za Amoni,
hata kwa dhambi nne, sitaizuia
ghadhabu yangu.
Kwa sababu aliwatumbua wanawake
wajawazito wa Gileadi
ili kuongeza mipaka yake.
14 [c]Nitatuma moto kwenye kuta za
Raba
ambao utateketeza ngome zake
katikati ya vilio vya vita katika siku
ya mapigano,
katikati ya upepo mkali katika
siku ya dhoruba.
15 [d]Mfalme wake atakwenda
uhamishoni,
yeye pamoja na maafisa wake,"
asema BWANA.

2 [e]Hili ndilo asemalo BWANA:

"Kwa dhambi tatu za
Moabu,
hata kwa dhambi nne, sitaizuia
ghadhabu yangu.
Kwa sababu alichoma mifupa ya
mfalme wa Edomu,
ikawa kama chokaa.
2 [f]Nitatuma moto juu ya Moabu
ambao utateketeza ngome za
Keriothi.
Moabu ataanguka kwa ghasia kubwa
katikati ya vilio vya vita na mlio
wa tarumbeta.
3 [g]Nitamwangamiza mtawala wake
na kuwaua maafisa wake wote
pamoja naye,"
asema BWANA.

4 [h]Hili ndilo asemalo BWANA:

"Kwa dhambi tatu za Yuda,
hata kwa dhambi nne, sitaizuia
ghadhabu yangu.
Kwa sababu wameikataa sheria ya
BWANA
na hawakuzishika amri zake,
kwa sababu wamepotoshwa na
miungu ya uongo,
miungu ambayo babu zao
waliifuata.
5 [i]Nitatuma moto juu ya Yuda
ambao utateketeza ngome za
Yerusalemu."

*Hukumu Juu Ya Israeli*

6 [j]Hili ndilo asemalo BWANA:

"Kwa dhambi tatu za Israeli,
hata kwa dhambi nne, sitaizuia
ghadhabu yangu.
Wanawauza wenye haki kwa fedha,
na maskini kwa jozi ya viatu.
7 [k]Wanakanyaga juu ya vichwa vya
maskini,
kama vile juu ya mavumbi ya
nchi,
na kukataa haki kwa walioonewa.

---

[a]**1:12** Mwa 36:11-15; Mao 1:9-10; Isa 34:5; 63:1-6; Eze 25:12-14; Mal 1:2-5
[b]**1:13** Mwa 19:38; 34:29; Yer 49:1-6; 2Fal 8:12; Hos 13:16; Eze 21:28
[c]**1:14** Kum 3:11; Ay 39:25; Eze 25:5; Amo 2:2; Isa 30:30; Yer 23:19
[d]**1:15** Yer 25:21; 49:1-3; Eze 21:28-32; 25:2-7; 1Nya 20:1
[e]**2:1** Eze 25:8; Sef 2:8; 2Fal 3:27; Isa 16:6; 33:2
[f]**2:2** Yer 48:7, 24; Ay 39:25; Yos 6:20
[g]**2:3** Hes 24:17; Za 2:10; Isa 40:23; Eze 25:8-11; Sef 2:8-9
[h]**2:4** Law 26:14; 2Sam 12:9, 10; 2Nya 36:14-17; Neh 1:7; Hos 12:2; Eze 9:11; Dan 9:11; 2Fal 17:19; Yer 6:19; 16:12; Isa 5:24; 9:16; 28:15; Kut 34:15
[i]**2:5** Yer 17:27; Hos 8:14; 2Fal 25:9; Amo 3:11; 2Nya 36:19
[j]**2:6** Isa 29:21; Yoe 3:3; Amo 5:11, 12; 8:6
[k]**2:7** Eze 36:20; 22:11; Law 18:21; 20:3; Amo 8:4; 5:11-12; Rum 2:24; Isa 10:2

Baba na mwanawe hushiriki
msichana mmoja,
kwa hivyo hulinajisi Jina langu
takatifu.
8 [a]Watu hulala kando ya kila
madhabahu
juu ya nguo zilizowekwa rehani.
Katika nyumba ya mungu wao
hunywa mvinyo
ulionunuliwa kwa fedha
walizotozwa watu.

9 [b]"Nilimwangamiza Mwamori mbele
yao,
ingawa alikuwa mrefu kama
mierezi,
na mwenye nguvu kama mialoni.
Niliyaangamiza matunda yake juu
na mizizi yake chini.

10 [c]"Niliwapandisha toka Misri,
na nikawaongoza miaka arobaini
jangwani
niwape nchi ya Waamori.
11 [d]Pia niliinua manabii kutoka
miongoni mwa wana wenu
na Wanadhiri kutoka miongoni
mwa vijana wenu.
Je, hii si kweli, enyi watu wa
Israeli?"
asema Bwana.
12 [e]"Lakini mliwafanya Wanadhiri
kunywa mvinyo
na kuwaamuru manabii wasitoe
unabii.

13 "Sasa basi, nitawaponda
kama gari lipondavyo wakati
limejazwa nafaka.
14 [f]Mkimbiaji hodari hatanusurika,
wenye nguvu wataishiwa nguvu
zao,
na shujaa hataweza kuokoa
maisha yake.
15 [g]Mpiga upinde atakimbia,
askari wapiga mbio hawataweza
kutoroka,
na mpanda farasi hataokoa maisha
yake.
16 [h]Hata askari walio mashujaa sana
siku hiyo watakimbia uchi,"
asema Bwana.

*Mashahidi Waitwa Dhidi Ya Israeli*

3 [i]Sikilizeni neno hili alilosema Bwana
dhidi yenu, enyi watu wa Israeli, dhidi
ya jamaa nzima niliowapandisha toka Misri:

2 [j]"Ni ninyi tu niliowachagua
kati ya jamaa zote za dunia;
kwa hiyo nitawaadhibu
kwa ajili ya dhambi zenu zote."

3 Je, watu wawili hutembea pamoja
wasipokubaliana kufanya hivyo?
4 [k]Je, simba hunguruma katika kichaka
wakati hana mawindo?
Aweza kuvuma katika pango
wakati ambao hajakamata
chochote?
5 Je, ndege aweza kuanguka kwenye
mtego ulio ardhini
ambapo hajategewa chambo?
Je, mtego unaweza kufyatuka toka
ardhini
wakati ambapo hakuna chochote
cha kunasa?

[a]**2:8** Kut 22:26; Hos 7:14; 1Kor 10:21; Hab 2:6; Amo 6:6; Kum 24:12-14
[b]**2:9** Hes 13:32; 21:23-26; Yos 10:12; Ay 18:16; Mal 4:1; Isa 10:33; Za 29:9
[c]**2:10** Kut 6:6; 20:2; Hes 21:23; Yos 13:4; Amo 9:7; Kum 8:2; 2:7
[d]**2:11** Kut 18:18; Yer 7:25; Hes 6:2-3; Amu 13:5
[e]**2:12** Mdo 4:18; Isa 30:10; Yer 11:21; Amo 7:12-13; Mik 2:6
[f]**2:14** 1Fal 20:11; Yer 9:23; Za 33:16; Ay 11:20; Isa 30:16-17
[g]**2:15** Eze 39:3; Kut 15:21; Zek 10:5; Mhu 9:11
[h]**2:16** Yer 48:41
[i]**3:1** Amo 2:10; Sef 2:5
[j]**3:2** Kut 19:6; 1Pet 4:17; Lk 12:47; Mik 2:3; Eze 9:6; Dan 9:12; Mt 11:22; Rum 2:9; Kum 7:6; Yer 14:10
[k]**3:4** Za 104:21; Hos 5:14; Isa 42:13

6 [a]Je, tarumbeta inapopigwa mjini
kujulisha hatari,
watu hawatetemeki?
Mji upatwapo na maafa,
je, si BWANA amesababisha?

7 [b]Hakika BWANA Mwenyezi hatafanya
neno lolote
bila kuwafunulia watumishi wake
manabii siri yake.

8 [c]Simba amenguruma:
je, ni nani ambaye hataogopa?
BWANA Mwenyezi ametamka:
je, ni nani awezaye kukosa kutoa
unabii?

9 [d]Tangazeni katika ngome za Ashdodi
na katika ngome za Misri:
"Kusanyikeni juu ya milima ya
Samaria;
angalieni wingi wa wasiwasi ulio
ndani yake,
na uonevu ulio miongoni mwa
watu wake."

10 [e]BWANA asema: "Hawajui kutenda
lililo jema,
wale ambao hujilundikia nyara
na vitu vilivyotekwa katika ngome
zao."

11 [f]Kwa hiyo hili ndilo asemalo BWANA
Mwenyezi:

"Adui ataizingira nchi;
ataangusha chini ngome zenu
na kuteka nyara maboma yenu."

12 [g]Hili ndilo asemalo BWANA:

"Kama vile mchungaji aokoavyo
kinywani mwa simba
vipande viwili tu vya mfupa wa
mguu
au kipande cha sikio,
hivyo ndivyo Waisraeli
watakavyookolewa,
wale wakaao Samaria
kwenye kingo za vitanda vyao,
na katika Dameski
kwenye viti vyao vya fahari."

13 "Sikia hili na ushuhudie dhidi ya
nyumba ya Yakobo," asema Bwana, BWANA
Mungu Mwenye Nguvu Zote.

14 [h]"Siku nitakapomwadhibu Israeli
kwa sababu ya dhambi zake,
nitaharibu madhabahu za Betheli;
pembe za madhabahu zitakatiliwa
mbali
na kuanguka chini.
15 [i]Nitabomoa nyumba ya wakati wa
masika,
pamoja na nyumba ya wakati wa
kiangazi;
nyumba zilizonakshiwa kwa pembe
za ndovu
na majumba makubwa ya fahari
yatabomolewa,"
asema BWANA.

*Israeli Hajarudi Kwa Mungu*

4 [j]Sikilizeni neno hili, ninyi ng'ombe
wa Bashani
mlioko juu ya Mlima Samaria,
ninyi wanawake mnaowaonea
maskini,
na kuwagandamiza wahitaji,
na kuwaambia wanaume wenu,
"Tuleteeni vinywaji!"

---

[a]**3:6** Isa 14:24-27; 31:2; 45:7; Hes 10:2; Eze 33:3; Ay 39:24; Yer 4:21
[b]**3:7** 1Sam 3:7; Mwa 6:13; 18:17; Mit 3:32; Yn 15:15; Yer 23:22; Mit 3:32; Dan 9:22-27; Ufu 1:1, 19
[c]**3:8** 1Kor 9:16; Yn 3:1-3; Mdo 4:20; Isa 31:4; 42:13; Yer 20:9
[d]**3:9** Yos 13:3; 2Nya 26:6
[e]**3:10** Yer 4:22; Amo 6:12; 5:7; Mik 6:10; Hab 2:8
[f]**3:11** Amo 2:5; 6:14; 2Fal 17:6
[g]**3:12** 1Sam 17:34; Es 1:6; Amo 6:4
[h]**3:14** Mwa 12:8; Amo 5:5-6; Kut 27:2; Law 26:18
[i]**3:15** Yer 36:22; Amu 3:20; 1Fal 22:39; Hos 10:5-8; Isa 34:5; Amo 5:11; 6:11
[j]**4:1** Za 22:12; Isa 58:6; Eze 39:18; 18:12; Amo 3:9; 2:8; 8:6; Yer 44:19

2 [a]BWANA Mwenyezi ameapa kwa
utakatifu wake:
"Hakika wakati utakuja
mtakapochukuliwa na kulabu,
na wanaosalia kwa ndoana za
samaki.
3 [b]Nanyi mtakwenda moja kwa moja
kupitia mahali palipobomolewa
kwenye ukuta,
nanyi mtatupwa nje kuelekea
Harmoni,"
asema BWANA.

4 [c]"Nendeni Betheli mkatende dhambi;
nendeni Gilgali mkazidi kutenda
dhambi.
Leteni dhabihu zenu kila asubuhi,
zaka zenu kila mwaka wa tatu.
5 Mchome mkate uliotiwa chachu
kama sadaka ya shukrani,
jisifuni kuhusu sadaka zenu za
hiari:
jigambeni kwa ajili ya sadaka hizo,
enyi Waisraeli,
kwa kuwa hili ndilo mnalopenda
kulitenda,"
asema BWANA Mwenyezi.

6 [d]"Niliwapa njaa kwenye kila mji,
na ukosefu wa chakula katika kila
mji,
hata hivyo bado hamjanirudia
mimi,"
asema BWANA.

7 [e]"Pia niliwazuilia ninyi mvua miezi
mitatu
kabla ya kufikia mavuno.
Nilinyesha mvua kwenye mji mmoja,
lakini niliizuia mvua isinyeshe mji
mwingine.
Shamba moja lilipata mvua,
na lingine halikupata, nalo
likakauka.
8 [f]Watu walitangatanga mji hata mji
kutafuta maji,
lakini hawakupata ya kuwatosha
kunywa,
hata hivyo hamjanirudia mimi,"
asema BWANA.

9 [g]"Mara nyingi nilizipiga bustani zenu
na mashamba ya mizabibu,
niliyapiga kwa kutu na ukungu.
Nzige walitafuna tini zenu na miti ya
mizeituni,
hata hivyo hamjanirudia mimi,"
asema BWANA.

10 [h]"Niliwapelekea tauni miongoni
mwenu
kama nilivyofanya kule Misri.
Niliwaua vijana wenu wa kiume kwa
upanga,
niliwachukua farasi wenu.
Nilijaza pua zenu kwa uvundo
kutoka kwenye kambi zenu,
hata hivyo hamjanirudia mimi,"
asema BWANA.

11 [i]"Niliwaangamiza baadhi yenu kama
nilivyoangamiza Sodoma na
Gomora.
Mlikuwa kama kijiti kiwakacho
kilichonyakuliwa motoni,
hata hivyo hamjanirudia,"
asema BWANA.

12 "Kwa hiyo hili ndilo
nitakalowafanyia, Israeli,
na kwa sababu nitawafanyia hili,
jiandaeni kukutana na Mungu
wenu, ee Israeli."

---

[a]**4:2** Amo 6:8; Isa 19:8; Yer 31:31; 2Fal 19:28; 2Nya 33:11
[b]**4:3** Eze 12:5
[c]**4:4** Hos 4:15; Hes 28:3, 4; 28:3; Eze 20:39; Kum 14:28; Yos 7:2; Amo 5:21, 22
[d]**4:6** Isa 9:13; 1Fal 17:1; Hag 2:17; Yer 5:3; Hos 5:15
[e]**4:7** Kum 11:17; Isa 5:6; Zek 14:17; Kut 9:4, 26; 2Nya 7:13
[f]**4:8** Eze 4:16-17; Ay 36:31; Yer 14:4; 2:7; Hag 1:6
[g]**4:9** Kum 28:22; Isa 9:13; Hag 2:17; Yer 3:10; Yoe 1:7; 2:25; Kut 10:13
[h]**4:10** Kut 9:3; 11:5; Kum 28:27; Isa 9:13, 17
[i]**4:11** Mwa 19:29; Yer 23:14; Isa 7:4; 13:19; Zek 3:2; Yud 23; Ay 36:13

13 [a]Yeye ambaye hufanya milima,
anaumba upepo,
na kufunua mawazo yake kwa mwanadamu,
yeye ageuzaye asubuhi kuwa giza,
na kukanyaga mahali pa juu pa nchi:
BWANA Mungu Mwenye Nguvu Zote ndilo jina lake.

*Maombolezo Na Wito Wa Toba*

5 [b]Sikia neno hili, ee nyumba ya Israeli, ombolezo hili ninalifanya kuwahusu ninyi:

2 [c]"Bikira Israeli ameanguka,
kamwe hatainuka tena,
ameachwa pweke katika nchi yake,
hakuna yeyote wa kumwinua."

3 [d]Hili ndilo BWANA Mwenyezi asemalo:

"Wakati mmoja wa miji yako
utakapopeleka watu elfu moja vitani kwa ajili ya Israeli,
mia moja tu watarudi;
wakati mji utakapopeleka mia moja,
kumi tu ndio watarudi hai."

4 [e]Hili ndilo BWANA asemalo kwa nyumba ya Israeli:

"Nitafuteni mpate kuishi;
5 [f]msitafute Betheli,
msiende Gilgali,
msisafiri kwenda Beer-Sheba.
Kwa maana kwa hakika Gilgali itakwenda uhamishoni,
na Betheli itafanywa kuwa si kitu."[g]

6 [h]Mtafuteni BWANA mpate kuishi,
au atafagia nyumba ya Yosefu kama moto;
utawateketeza, nayo Betheli
haitakuwa na yeyote wa kuuzima.

7 [i]Ninyi ambao mnageuza haki kuwa uchungu
na kuiangusha haki chini
8 [j](yeye ambaye alifanya Kilimia na Orioni,
ambaye hugeuza giza kuwa mapambazuko
na mchana kuwa usiku,
ambaye huyaita maji ya bahari
na kuyamwaga juu ya uso wa nchi:
BWANA ndilo jina lake;
9 yeye hufanya maangamizo kwenye ngome
na kufanya mji uliozungushiwa ngome kuwa ukiwa),
10 [k]mnamchukia yule akemeaye mahakamani,
na kumdharau yule ambaye husema kweli.

11 [l]Mnamgandamiza maskini
na kumlazimisha awape nafaka.
Kwa hiyo, ingawa mmejenga
majumba ya mawe ya fahari,
hamtaishi ndani yake;
ingawa mmepanda mashamba
mazuri ya mizabibu,
hamtakunywa divai yake.
12 [m]Kwa kuwa ninajua hesabu ya makosa yenu
na ukubwa wa dhambi zenu.

---

[a]**4:13** Dan 2:28; Za 65:6; 135:7; Yn 2:25; Amo 9:6; 5:8, 27; Isa 47:4
[b]**5:1** Yer 4:8; 7:29; Eze 9:1
[c]**5:2** 2Fal 19:21; Yer 14:17; 50:32; Amo 8:14
[d]**5:3** Amo 6:9; Isa 6:13
[e]**5:4** Kum 32:46-47; 4:29; Isa 55:3; 2Nya 15:2; Yer 29:13; Eze 18:9
[f]**5:5** 1Sam 11:14; 7:16; 8:6; Mwa 21:31; Hos 4:15; Amu 8:14
[g]5 Yaani *Aveni* kwa Kiebrania, kumaanisha Beth-Aveni, jina lingine la Betheli kwa dhihaka.
[h]**5:6** Sef 2:3; Amo 3:14; Law 18:5; Za 22:26; 105:4; Kum 4:24
[i]**5:7** Isa 5:20; Amo 6:12; 3:10; Hos 10:4
[j]**5:8** Ay 38:31-34; Mwa 1:16; Isa 42:16; Za 104:6-9, 20; Yer 16:21; Amo 4:13
[k]**5:10** Isa 29:21; Mwa 4:16; 1Fal 22:8; Gal 4:16
[l]**5:11** Mik 6:15; Amo 8:6; 3:15; 9:14; Amu 9:27; Sef 1:13
[m]**5:12** Ay 5:4; 36:18; Isa 29:21; 5:23; 1:23; Hos 5:3; Eze 22:12; Yer 5:28; Amo 2:6-7

Mmewaonea wenye haki na kupokea
rushwa
na kuzuia haki ya maskini
mahakamani.
13 Kwa hiyo mtu mwenye busara
hunyamaza kimya nyakati
kama hizo,
kwa kuwa nyakati ni mbaya.

14 [a]Tafuteni mema, wala si mabaya,
ili mpate kuishi.
Ndipo BWANA Mungu Mwenye
Nguvu Zote atakuwa pamoja
nanyi,
kama msemavyo yupo nanyi.
15 [b]Yachukieni maovu, yapendeni
mema;
dumisheni haki mahakamani.
Yamkini BWANA Mungu Mwenye
Nguvu Zote
atawahurumia mabaki ya Yosefu.

16 [c]Kwa hiyo hili ndilo Bwana, BWANA
Mungu Mwenye Nguvu Zote, asemalo:

"Kutakuwepo maombolezo katika
barabara zote
na vilio vya uchungu katika njia
kuu zote.
Wakulima wataitwa kuja kulia,
na waombolezaji waje
kuomboleza.
17 [d]Kutakuwepo kuomboleza katika
mashamba yote ya mizabibu,
kwa kuwa nitapita katikati yenu,"
asema BWANA.

*Siku Ya BWANA*

18 [e]Ole wenu ninyi mnaoitamani
siku ya BWANA!
Kwa nini mnaitamani siku ya
BWANA?
Siku hiyo itakuwa giza, si nuru.

19 [f]Itakuwa kama vile mtu
aliyemkimbia simba
kumbe akakutana na dubu,
kama vile mtu aliyeingia nyumbani
mwake
na kuupumzisha mkono wake
kwenye ukuta,
kumbe akaumwa na nyoka.
20 [g]Je, siku ya BWANA haitakuwa giza,
na si nuru:
giza nene, bila mwonzi wa
mwanga?

21 [h]"Ninachukia, ninazidharau sikukuu
zenu za dini;
siwezi kuvumilia makusanyiko
yenu.
22 [i]Hata ingawa mnaniletea sadaka
zenu za kuteketezwa na
sadaka za nafaka,
sitazikubali.
Ingawa mnaniletea sadaka nzuri za
amani,
sitazitambua.
23 Niondoleeni kelele za nyimbo zenu!
Sitasikiliza sauti za vinubi vyenu.
24 [j]Lakini acheni haki itiririke kama
mto,
na uadilifu uwe kama kijito
kisichokauka!

25 [k]"Je, mliniletea dhabihu na sadaka
kwa miaka arobaini kule
jangwani,
ee nyumba ya Israeli?
26 [l]Mmeyainua madhabahu ya mfalme
wenu,
Sikuthi mungu wenu mtawala,

---

[a]**5:14** Za 34:12-16; Mit 7:7; 11:27; Isa 1:16, 17; Mik 3:11; 6:8; Rum 2:7-9
[b]**5:15** Rum 12:9; Yoe 2:14; Kut 32:30; Za 52:3; 97:10; Mik 5:7-8; 7:18; Mwa 18:25
[c]**5:16** Yer 9:17; 7:34; Sef 1:10; Yoe 1:11
[d]**5:17** Kut 12:12; Isa 16:10; Yer 48:33
[e]**5:18** Isa 2:12; 5:19, 30; Yoe 1:15; Ay 20:28; Yer 30:7; 1Sam 2:9
[f]**5:19** Mhu 10:8; Kum 32:34; Ay 20:24; Mao 3:10; Eze 12:22; Mal 3:1; 2Pet 3:4; Isa 24:17-18; Yer 15:2-3
[g]**5:20** Oba 1:15; Eze 7:7; 1Sam 2:9; Isa 13:10; Sef 1:15
[h]**5:21** Law 26:31; Hos 2:11; Yer 44:4; Isa 1:11-16; Eze 23:18
[i]**5:22** Yer 14:12; 7:21; Mik 6:6-7; Isa 1:11-16; 66:3; Za 40:6; Amo 4:4
[j]**5:24** Yer 22:3; Mik 6:8; Isa 45:8
[k]**5:25** Isa 43:23; Mdo 7:42; Kum 32:17; Kut 16:35
[l]**5:26** Eze 18:6; 20:16

na Kiuni mungu wenu wa nyota,
ambao mliwatengeneza wenyewe.
27 [a]Kwa sababu hiyo nitawapeleka
uhamishoni mbali kupita
Dameski,”
asema BWANA, ambaye jina lake
ni Mungu Mwenye Nguvu
Zote.

*Ole Kwa Wanaoridhika*

6 [b]Ole wenu ninyi mnaostarehe na
kuridhika katika Sayuni,
na ninyi mnaojisikia salama juu ya
Mlima Samaria,
ninyi watu mashuhuri wa taifa
lililoendelea kuliko mataifa
mengine,
ambao watu wa Israeli
wanawategemea!
2 [c]Nendeni Kalne mkaone kutoka huko;
mwende hadi Hamathi iliyo kuu,
kisha mshuke hadi Gathi ya
Wafilisti.
Je, wao ni bora kuliko falme zenu
mbili?
Je, nchi yao ni kubwa kuliko
yenu?
3 [d]Mnaiweka mbali siku iliyo mbaya
na kuleta karibu utawala wa
kuogofya.
4 [e]Ninyi mnalala juu ya vitanda
vilivyofunikwa kwa pembe za
ndovu,
na kujinyoosha juu ya viti vya
fahari.
Mnajilisha kwa wana-kondoo wazuri
na ndama walionenepeshwa.
5 [f]Ninyi mnapiga vinubi kama Daudi,
huku mkitunga nyimbo za vinanda
mbalimbali.
6 [g]Mnakunywa mvinyo kwa bakuli
zilizojazwa,
na mnajipaka mafuta mazuri,
lakini hamhuzuniki kwa
maangamizi ya Yosefu.
7 Kwa hiyo mtakuwa miongoni mwa
watu wa kwanza kwenda
uhamishoni;
karamu zenu na kustarehe
kutakoma.

*BWANA Anachukia Kiburi Cha Israeli*

8 [h]BWANA Mwenyezi ameapa kwa nafsi
yake mwenyewe: BWANA Mungu Mwenye
Nguvu Zote asema:

“Nachukia kiburi cha Yakobo,
nachukia ngome zake;
nitautoa mji wao na kila kitu
kilichomo ndani mwake.”

9 Kama watu kumi watabaki katika
nyumba moja, wao pia watakufa. 10 [i]Kama
jamaa ambaye atachoma miili akija ili
kuitoa nje ya nyumba, na kumuuliza
yeyote ambaye bado anajificha humo,
“Je, yuko mtu yeyote pamoja nawe?” Naye
akisema, “Hapana,” ndipo atakaposema,
“Nyamaza kimya! Haturuhusiwi kutaja jina
la BWANA.”

11 [j]Kwa kuwa BWANA ameamuru,
naye atabomoa jumba kubwa
vipande vipande
na nyumba ndogo vipande vidogo
vidogo.

12 [k]Je, farasi waweza kukimbia kwenye
miamba mikali?
Je, aweza mtu kulima huko kwa
maksai?

---

[a]**5:27** Yer 38:17; Amo 6:7; Mdo 7:42-43; Mik 1:16; Kum 32:17-19
[b]**6:1** Lk 6:24; Isa 32:9-11; Ay 24:23; Sef 1:12; Amo 3:9
[c]**6:2** 2Fal 17:24; Yer 49:23; Isa 10:9; 2Fal 14:25; Hes 34:8; Mwa 10:10; 2Nya 26:6; Yos 11:22
[d]**6:3** Isa 47:7; 56:12; Eze 12:22, 27; Mhu 8:11; Amo 5:18; 9:10
[e]**6:4** Isa 1:11; Eze 34:2-3; Amo 3:12; Mit 3:12; 7:17; Es 1:6
[f]**6:5** Isa 5:12; 14:11; Za 137:2; Amo 5:23; 1Nya 15:16
[g]**6:6** Isa 28:1; Amo 2:8; Eze 9:4; 16:49
[h]**6:8** Mwa 22:16; Ebr 6:13; Law 26:19, 30; Za 47:4; Kum 32:19; Yer 12:8; Amo 4:2
[i]**6:10** 1Sam 31:12; Amo 8:3
[j]**6:11** Amo 3:15; Isa 55:11; 34:5
[k]**6:12** Hos 10:4; Isa 1:21; Amo 5:7; 3:10

Lakini mmegeuza haki kuwa sumu
na matunda ya uadilifu kuwa uchungu:
13 [a]ninyi mnaoshangilia kushindwa kwa Lo-Debari
na kusema, "Je, hatukuteka Karnaimu kwa nguvu zetu wenyewe?"

14 [b]Maana BWANA Mungu Mwenye Nguvu Zote asema,
"Nitainua taifa dhidi yenu, ee nyumba ya Israeli,
nalo litawatesa kuanzia Lebo-Hamathi
hadi Bonde la Araba."

*Maono Ya Kwanza: Nzige*

7 [c]Hili ndilo alilonionyesha BWANA
Mwenyezi katika maono: Alikuwa
anaandaa makundi ya nzige baada ya
kuvunwa fungu la mfalme na wakati ule
tu mimea ya pili ilipokuwa ikichipua.
2 [d]Wakati nzige walikuwa wamekula mimea
yote ya nchi, nililia kwa sauti kuu, "BWANA
Mwenyezi, samehe! Je, Yakobo atawezaje
kuendelea kuishi? Yeye ni mdogo sana!"
3 [e]Kwa hiyo BWANA akaghairi.
Kisha BWANA akasema, "Hili halitatokea."

*Maono Ya Pili: Moto*

4 [f]Hili ndilo BWANA Mwenyezi
alilonionyesha katika maono: BWANA
Mwenyezi alikuwa akiita hukumu ya moto;
nao ulikausha vilindi vikuu, ukateketeza
nchi. 5 [g]Ndipo nikalia, "BWANA Mwenyezi,
nakusihi, zuia! Je, Yakobo atawezaje
kuendelea kuishi? Yeye ni mdogo sana!"
6 [h]Kwa hiyo BWANA akaghairi.
BWANA Mwenyezi akasema, "Hili nalo halitatokea."

*Maono Ya Tatu: Timazi*

7 Hili ndilo alilonionyesha katika maono:
Bwana alikuwa amesimama karibu na ukuta
ambao ulikuwa umejengwa kwa timazi,
akiwa na uzi wa timazi mkononi mwake.
8 [i]Naye BWANA akaniuliza, "Je, Amosi
unaona nini?"
Nikamjibu, "Uzi wa timazi."
Kisha Bwana akasema, "Tazama, ninaweka uzi wa timazi miongoni mwa watu wangu Israeli; sitawahurumia tena.

9 [j]"Mahali pa Isaki pa juu pa kuabudia miungu pataangamizwa,
na mahali patakatifu pa Israeli pa kuabudia pataharibiwa;
kwa upanga wangu nitainuka
dhidi ya nyumba ya Yeroboamu."

*Amosi Na Amazia*

10 [k]Kisha Amazia kuhani wa Betheli
akatuma ujumbe kwa Yeroboamu mfalme
wa Israeli, akisema: "Amosi analeta fitina
juu yako katikati ya Israeli. Nchi haiwezi
kuvumilia maneno yake yote. 11 [l]Kwa kuwa
hili ndilo Amosi analosema:

" 'Yeroboamu atakufa kwa upanga,
na kwa hakika Israeli watakwenda uhamishoni,
mbali na nchi yao.' "

12 [m]Kisha Amazia akamwambia Amosi,
"Nenda zako, ewe mwonaji! Urudi katika
nchi ya Yuda. Ujipatie riziki yako huko na
kutoa unabii wako. 13 [n]Usiendelee kutoa
unabii katika Betheli, kwa sababu hapa ni
mahali pa mfalme pa kuabudia na Hekalu
la ufalme huu."

[a]**6:13** Ay 13:8; 8:15; Isa 28:14-15
[b]**6:14** Yer 5:15; Hes 13:21; 1Fal 8:65; Amo 3:11
[c]**7:1** Amo 8:1; Za 78:46; Yer 51:14; Yoe 1:4
[d]**7:2** Kut 10:15; Eze 11:13; Isa 37:4; Amo 4:9
[e]**7:3** Kut 32:14; Yon 3:10; Kum 32:36; Za 106:45; 1Nya 21:15; Hos 11:8; Yoe 2:14; Yak 5:16; Yer 18:8; 26:19
[f]**7:4** Isa 66:16; Yoe 1:19; Kum 32:22
[g]**7:5** Yoe 2:17
[h]**7:6** Kut 32:14; Yer 18:8; 42:10; Za 102:17; Yon 3:10; Eze 9:8
[i]**7:8** Isa 28:17; Mao 2:8; 2Fal 21:13; Eze 7:2-9; Yer 1:11-13; 15:6; Mik 7:18
[j]**7:9** Law 26:31; Mwa 26:23; 2Fal 14:23; 1Fal 13:34; 2Fal 15:9-10; Isa 63:18; Hos 10:8
[k]**7:10** 1Fal 12:32; Yos 7:2; 2Fal 14:23-24; Yer 38:4; 26:8-11
[l]**7:11** Amo 5:27; Yer 36:16
[m]**7:12** Mt 8:34; 1Sam 9:9
[n]**7:13** Yer 20:2; 36:5; Amo 2:12; Mdo 4:18; Yos 7:2; 1Fal 12:29

14 [a]Amosi akamjibu Amazia, “Mimi
sikuwa nabii wala mwana wa nabii,
lakini nilikuwa mchungaji wa kondoo na
mtunza mikuyu. 15 [b]Lakini BWANA akanitoa
kutoka kuchunga kondoo na kuniambia,
‘Nenda, ukawatabirie watu wangu Israeli.’
16 [c]Sasa basi, sikieni neno la BWANA. Ninyi
mnasema,

“ ‘Usitabiri dhidi ya Israeli,
na uache kuhubiri dhidi ya
nyumba ya Isaki.’

17 [d]“Kwa hiyo hili ndilo asemalo BWANA:

“ ‘Mke wako atakuwa kahaba mjini,
nao wana wako na binti zako
watauawa kwa upanga.
Shamba lako litapimwa na
kugawanywa,
na wewe mwenyewe utafia katika
nchi ya kipagani.
Nayo Israeli kwa hakika itakwenda
uhamishoni,
mbali na nchi yao.’ ”

*Maono Ya Nne: Kikapu Cha Matunda Yaliyoiva*

8 Hili ndilo alilonionyesha BWANA
Mwenyezi katika maono: kikapu cha
matunda yaliyoiva. 2 [e]Akaniuliza, “Amosi,
unaona nini?”

Nikajibu, “Kikapu chenye matunda
yaliyoiva.”

Ndipo BWANA akaniambia, “Wakati
umewadia kwa watu wangu Israeli;
sitawahurumia zaidi.”

3 [f]BWANA Mwenyezi asema, “Katika siku
ile, nyimbo katika Hekalu zitageuka kuwa
maombolezo. Miili mingi, mingi sana:
itatupwa kila mahali! Kimya!”

4 [g]Lisikieni hili, ninyi ambao
mnawagandamiza wahitaji,
na kuwaonea maskini wa nchi,

5 [h]mkisema,

“Ni lini Mwezi Mwandamo
utakapopita
ili tupate kuuza nafaka,
na Sabato itakwisha lini
ili tuweze kuuza ngano?”
Mkipunguza vipimo,
na kuongeza bei,
na kudanganya kwa mizani zisizo
sawa,
6 [i]mkiwanunua maskini kwa fedha,
na wahitaji kwa jozi ya viatu,
na mkiuza hata takataka za ngano
pamoja na ngano.

7 [j]BWANA ameapa kwake mwenyewe,
aliye Kiburi cha Yakobo: “Kamwe sitasahau
chochote ambacho wamefanya.

8 [k]“Je, nchi haitatetemeka kwa ajili ya
hili,
nao wote waishio ndani mwake
hawataomboleza?
Nchi yote itainuka kama Naili;
itapanda na kushuka kama mto wa
Misri.

9 [l]“Katika siku ile,” asema BWANA
Mwenyezi,

“Nitalifanya jua litue alasiri na
kuifanya dunia
iwe giza wakati wa mchana
mwangavu.

[a]**7:14** 1Sam 10:5; Zek 13:5; 2Fal 2:5; 4:38; Isa 9:10; 1Fal 10:27
[b]**7:15** Mwa 37:5; 2Sam 7:8; Yer 7:1-2; 26:12; Eze 2:3-4; Isa 6:9
[c]**7:16** Isa 30:10; Eze 20:46; Mik 2:6; Yer 22:2
[d]**7:17** Hos 4:13; 9:3; Eze 4:13; Yer 28:12; 29:21; Mao 5:11; Amo 5:27; 2:12-13; 2Fal 17:6
[e]**8:2** Mao 4:18; Yer 1:2, 13; 24:3; Eze 7:2-9; Amo 7:8; Mwa 40:16
[f]**8:3** Amo 5:16-23; 6:10
[g]**8:4** Mit 30:14; Ay 20:19; Zek 14:4; Amo 2:7
[h]**8:5** Kum 25:15; 2Fal 4:23; Neh 13:15-16; Hes 10:10; Isa 58:13; Mik 6:10; Mwa 31:7; Hos 12:7
[i]**8:6** Amo 2:6; 4:1; 5:11
[j]**8:7** Hos 8:13; Amo 6:8; Za 47:4; 68:34; Ay 35:15
[k]**8:8** Ay 9:6; Hos 4:3; Yer 46:8; 51:29; Za 18:7; Amo 9:5
[l]**8:9** Ay 5:14; Mk 15:33; Eze 32:7; Amo 4:13; 5:8; Isa 13:10; 59:9-10; Yer 15:9; Mik 3:6; 1The 5:2, 3; Mt 27:45

10 [a]Nitageuza sikukuu zenu za kidini
kuwa maombolezo,
na kuimba kwenu kote kuwe kilio.
Nitawafanya ninyi nyote mvae nguo
ya gunia
na kunyoa nywele zenu.
Nitaufanya wakati ule uwe kama
wa kuombolezea mwana wa
pekee,
na mwisho wake kama siku ya
uchungu.

11 [b]"Siku zinakuja," asema BWANA
Mwenyezi,
"wakati nitakapotuma njaa katika
nchi yote:
si njaa ya chakula wala kiu ya maji,
lakini njaa ya kusikia maneno ya
BWANA.
12 [c]Wanaume watayumbayumba kutoka
bahari hadi bahari
na kutangatanga kutoka kaskazini
mpaka mashariki,
wakitafuta neno la BWANA,
lakini hawatalipata.

13 [d]"Katika siku ile

"wasichana wazuri na vijana
wanaume wenye nguvu
watazimia kwa sababu ya kiu.
14 Wale waapao kwa aibu ya Samaria,
au kusema, 'Hakika kama miungu
yenu iishivyo, ee Dani,'
au 'Hakika kama mungu wa Beer-
Sheba aishivyo':
wataanguka, wala hawatasimama
tena."

*Israeli Kuangamizwa*

9 [e]Nilimwona Bwana akiwa amesimama
kando ya madhabahu, naye akasema:

"Piga vichwa vya nguzo
ili vizingiti vitikisike.
Viangushe juu ya vichwa vya watu
wote;
na wale watakaosalia nitawaua
kwa upanga.
Hakuna awaye yote atakayekimbia,
hakuna atakayetoroka.
2 [f]Wajapojichimbia chini mpaka
kwenye vina vya kuzimu,
kutoka huko mkono wangu
utawatoa.
Wajapopanda juu hadi kwenye
mbingu,
kutoka huko nitawashusha.
3 [g]Wajapojificha juu ya kilele cha
Karmeli,
huko nitawawinda na
kuwakamata.
Wajapojificha kutoka kwenye uso
wangu
katika vilindi vya bahari,
huko nako nitaamuru joka
kuwauma.
4 [h]Wajapopelekwa uhamishoni na adui
zao,
huko nako nitaamuru upanga
uwaue.
Nitawakazia macho yangu kwa
mabaya
wala si kwa mazuri."

5 [i]Bwana, BWANA Mwenye Nguvu
Zote,
yeye agusaye dunia nayo
ikayeyuka,
na wote wakaao ndani mwake
wakaomboleza:
nayo nchi yote huinuka kama Naili,
kisha hushuka kama mto wa Misri;

---

[a]**8:10** Yoe 1:8; Zek 12:10; Mwa 21:16; Hos 2:11; Lk 7:12, 13; Yer 6:26; 48:37; 2:19; Eze 7:18; Law 26:31; 13:40; Mao 5:15; Isa 3:17
[b]**8:11** 1Sam 3:1; 28:6; Eze 7:26; Za 74:9; Mik 3:6; 2Nya 15:3; Yer 30:3; 31:27
[c]**8:12** Eze 20:31
[d]**8:13** Isa 41:17; 9:17; Hos 2:3; 8:14; Kum 9:21; 1Fal 12:29, 30; Hos 8:5, 6; 10:5; Mik 1:5; Za 46:2; Amo 5:2-5
[e]**9:1** Za 68:21; Yer 11:11
[f]**9:2** Za 139:8-10; Ay 20:6; 7:9; Yer 51:33; Oba 1:4; Eze 26:20
[g]**9:3** Yer 23:24; 6:16-17; Za 139:8-10; 68:22; Mwa 49:17; Ay 11:20
[h]**9:4** Law 26:33; 17:10; Eze 5:12; 15:7; Kum 28:65; Yer 39:16; 21:10; 44:11
[i]**9:5** Za 46:2; Amo 8:8; Mik 1:4

6 [a]yeye ambaye hujenga jumba lake la
kifalme katika mbingu
na kuisimika misingi yake juu ya
dunia,
yeye aitaye maji ya bahari
na kuyamwaga juu ya uso wa
nchi:
BWANA ndilo jina lake.

7 [b]"Je, Waisraeli,
ninyi si sawa kwangu kama
Wakushi?"
asema BWANA.
"Je, sikuleta Israeli kutoka Misri,
Wafilisti kutoka Kaftori,[c]
na Washamu kutoka Kiri?

8 [d]"Hakika macho ya BWANA
Mwenyezi
yako juu ya ufalme wenye
dhambi.
Nami nitauangamiza
kutoka kwenye uso wa dunia:
hata hivyo sitaiangamiza kabisa
nyumba ya Yakobo,"
asema BWANA.
9 [e]"Kwa kuwa nitatoa amri,
na nitaipepeta nyumba ya Israeli
miongoni mwa mataifa yote,
kama vile nafaka ipepetwavyo katika
ungo,
na hakuna hata punje moja
itakayoanguka chini.
10 [f]Watenda dhambi wote miongoni
mwa watu wangu
watauawa kwa upanga,
wale wote wasemao,
'Maafa hayatatupata wala
kutukuta.'

*Kurejezwa Kwa Israeli*

11 [g]"Katika siku ile nitaisimamisha
hema ya Daudi iliyoanguka.
Nitakarabati mahali palipobomoka
na kujenga upya magofu yake,
na kuijenga kama ilivyokuwa
awali,
12 [h]ili wapate kuyamiliki mabaki ya
Edomu,
na mataifa yote yale yanayobeba
Jina langu,"
asema BWANA ambaye atafanya
mambo haya.

13 [i]"Siku zinakuja," asema BWANA,

"wakati mvunaji atatanguliwa na
mkulima,
naye mpanzi atatanguliwa na yeye
akamuaye zabibu.
Divai mpya itadondoka kutoka
milimani,
na kutiririka kutoka vilima vyote.
14 [j]Nitawarejesha tena watu wangu
Israeli waliohamishwa;
wataijenga tena miji iliyoachwa
magofu,
nao wataishi ndani mwake.
Watapanda mizabibu na kunywa
divai yake;
watalima bustani na kula matunda
yake.
15 [k]Nitaipanda Israeli katika nchi yao
wenyewe,
hawatang'olewa tena
kutoka nchi ambayo nimewapa,"

asema BWANA Mungu wenu.

---

[a]**9:6** Za 104:1-3, 5-13; Amo 5:8; Yer 43:9
[b]**9:7** 2Nya 12:3; Kum 2:23; Isa 43:3; 22:6; 2Fal 16:9; Yer 47:4; Amo 1:5; Mwa 10:14
[c]7 Yaani Krete.
[d]**9:8** Yer 30:11; 44:27; Za 11:4
[e]**9:9** Lk 22:31; Isa 30:28; Yer 31:36; Dan 9:7
[f]**9:10** Yer 5:12; 23:17; 49:37; Eze 20:38; Amo 6:3
[g]**9:11** Mdo 15:16; Mik 7:8-11; Zek 12:7; Isa 7:2; 49:8; Mwa 26:22; Eze 17:24
[h]**9:12** Hes 24:18; Isa 43:7; Oba 1:19; Yer 25:29; Mdo 15:16-17
[i]**9:13** Law 26:5; Amu 9:27; Yoe 3:18; 2:24; Yer 31:38; 33:14; Rut 2:3
[j]**9:14** Isa 32:18; 49:8; 62:9; 61:4; Eze 34:13-14; Yer 29:14; 33:7; 30:18
[k]**9:15** Kut 15:17; Isa 60:21; 65:9; Yer 18:9; 23:8; 3:18; 24:6; 32:15; Eze 28:26; 34:28; Yoe 3:20

# OBADIA

1 [a]Maono ya Obadia.

Hili ndilo asemalo Bwana Mwenyezi kuhusu Edomu:

Tumesikia ujumbe kutoka kwa
Bwana:
Mjumbe alitumwa kwa mataifa
kusema,
"Inukeni, twendeni tukapigane vita
dhidi yake."

2 "Angalieni, nitawafanya wadogo
miongoni mwa mataifa,
mtadharauliwa kabisa.
3 [b]Kiburi cha moyo wako
kimekudanganya,
wewe unayeishi katika majabali ya
miamba
na kufanya makao yako juu,
wewe unayejiambia mwenyewe,
'Ni nani awezaye kunishusha
chini?'
4 [c]Ingawa unapaa juu kama tai
na kufanya kiota chako kati ya
nyota,
nitakushusha chini kutoka huko,"
asema Bwana.
5 [d]"Ikiwa wevi wangekuja kwako,
ikiwa wanyang'anyi wangekujia
usiku:
Lo! Tazama ni maafa kiasi gani
yangekuwa yanakungojea:
je, si wangeiba tu kiasi ambacho
wangehitaji?
Kama wachuma zabibu wangekuja
kwako,
je, wasingebakiza zabibu chache?
6 Lakini tazama jinsi Esau
atakavyotekwa,
jinsi hazina zake zilizofichwa
zitatekwa nyara!
7 [e]Wote ulioungana nao watakufukuza
hadi mpakani,
rafiki zako watakudanganya na
kukushinda,
wale wanaokula mkate wako
watakutegea mtego,
lakini hutaweza kuugundua.

8 [f]"Katika siku hiyo," asema Bwana,
"je, sitaangamiza watu wenye
hekima wa Edomu,
watu wenye ufahamu katika
milima ya Esau?
9 [g]Ee Temani, mashujaa wako
watatiwa hofu,
kila mmoja katika milima ya Esau
ataangushwa chini kwa kuchinjwa.
10 [h]Kwa sababu ya jeuri uliyofanya
dhidi ya ndugu yako Yakobo,
aibu itakufunika;
utaangamizwa milele.
11 [i]Siku ile ulisimama mbali ukiangalia
wakati wageni walipojichukulia
utajiri wake
na watu wa nchi nyingine
walipoingia malango yake
wakipiga kura kwa ajili ya
Yerusalemu,
ulikuwa kama mmoja wao.
12 [j]Usingemdharau ndugu yako
katika siku ya msiba wake,
wala kufurahia juu ya watu wa Yuda
katika siku ya maangamizi yao,

[a]**1:1** Mwa 25:14; Isa 1:1; 21:11; Yoe 3:19; Mal 1:3; Eze 25:12-14; Yer 6:4-5; 49:7-22; Isa 11:14; 18:2; 34:11
[b]**1:3** Isa 14:13; 16:6; 2Fal 14:7; 2Nya 25:11-12; Ufu 18:7
[c]**1:4** Isa 10:14; 14:13; 14:14, 15; Ay 20:6; Amo 9:2; Yer 49:16; Hab 2:9
[d]**1:5** Isa 24:13; Kum 4:27; 24:21
[e]**1:7** Yer 30:14; Za 41:9
[f]**1:8** Ay 5:12; Isa 29:14
[g]**1:9** Mwa 36:11, 34; Amo 2:16; Za 76:5; Yer 49:22; Nah 3:13
[h]**1:10** Yoe 3:19; Amo 1:11-12; Za 137:7; Mwa 47:21; Eze 35:5, 15; Mal 1:4; Eze 25:12-14; 35:9
[i]**1:11** Ay 6:27; Nah 3:10; Eze 24:6
[j]**1:12** Eze 25:6; 35:15; Mit 17:5; 24:17; Mik 4:11; Ay 31:29

wala kujigamba sana
katika siku ya taabu yao.
13 [a]Usingeingia katika malango ya watu wangu
katika siku ya maafa yao,
wala kuwadharau katika janga lao
katika siku ya maafa yao,
wala kunyang'anya mali zao
katika siku ya maafa yao.
14 Usingengoja kwenye njia panda
na kuwaua wakimbizi wao,
wala kuwatoa watu wake waliosalia
katika siku ya shida yao.

15 [b]"Siku ya BWANA iko karibu
kwa mataifa yote.
Kama ulivyofanya, nawe utafanyiwa vivyo hivyo,
matendo yako yatakurudia juu ya kichwa chako.
16 [c]Kama vile ulivyokunywa juu ya mlima wangu mtakatifu,
vivyo hivyo mataifa yote watakunywa mfululizo,
watakunywa na kunywa,
nao watatoweka kana kwamba hawajawahi kuwepo.
17 [d]Lakini katika Mlima Sayuni kutakuwepo
na wale watakaookoka;
nao utakuwa mtakatifu,
nayo nyumba ya Yakobo
itamiliki urithi wake.
18 [e]Nyumba ya Yakobo itakuwa moto,
na nyumba ya Yosefu itakuwa mwali wa moto;
nayo nyumba ya Esau itakuwa bua kavu,
nao wataiwasha moto na kuiteketeza.
Hakutakuwa na watakaosalimika
kutoka nyumba ya Esau."
BWANA amesema.
19 [f]Watu kutoka nchi ya Negebu
wataikalia milima ya Esau,
na watu kutoka miteremko ya vilima
watamiliki nchi ya Wafilisti.
Watayakalia mashamba ya Efraimu na Samaria,
naye Benyamini atamiliki Gileadi.
20 [g]Kundi la Waisraeli walioko uhamishoni Kanaani
watarudi na kumiliki nchi mpaka Sarepta.
Walioko uhamishoni Sefaradi kutoka Yerusalemu
watamiliki miji ya Negebu.
21 [h]Waokoaji watakwea juu ya Mlima Sayuni
kutawala milima ya Esau.
Nao ufalme utakuwa wa BWANA.

---

[a]**1:13** Eze 35:5
[b]**1:15** Yer 46:10; 50:29; Hab 2:8; Amu 1:7; Za 137:8; Eze 35:15; Yoe 2:31; 3:7-8; Eze 30:3; Amo 5:8
[c]**1:16** Yer 25:15; 49:12; Mao 4:21-22; Isa 51:17; Kut 15:17; Eze 25:12-14
[d]**1:17** Za 69:35; 74:2; Isa 14:1-2; Amo 9:11-15; Zek 8:12
[e]**1:18** Zek 12:6; Yer 49:10; Isa 1:31
[f]**1:19** Isa 11:14; Sef 2:7; Yer 31:5; Hes 1:36
[g]**1:20** Lk 4:26; Yer 33:13; 1Fal 17:9-10
[h]**1:21** Dan 2:24, 44; Ufu 11:15; Zek 14:9; Isa 19:20; Amu 3:9; Za 22:28; 47:9

# YONA

*Yona Anamkimbia Bwana*

1 [a]Neno la Bwana lilimjia Yona mwana
wa Amitai: 2 [b]"Nenda katika mji mkubwa
wa Ninawi ukahubiri juu yake, kwa sababu
uovu wake umekuja juu mbele zangu."
3 [c]Lakini Yona alimkimbia Bwana na
kuelekea Tarshishi. Alishuka mpaka Yafa,
ambapo alikuta meli iliyokuwa imepangwa
kuelekea bandari ile. Baada ya kulipa nauli,
akapanda melini na kuelekea Tarshishi
ili kumkimbia Bwana. 4 [d]Ndipo Bwana
akatuma upepo mkali baharini, nayo
dhoruba kali sana ikavuma hata meli
ikawa hatarini kuvunjika. 5 [e]Mabaharia
wote waliogopa na kila mmoja akamlilia
mungu wake mwenyewe. Nao wakatupa
mizigo baharini ili meli ipungue uzito.
Lakini Yona alikuwa ameteremkia
chumba cha ndani ya meli, mahali ambapo
alilala na kupatwa na usingizi mzito.
6 [f]Nahodha akamwendea na kusema, "Wewe
unawezaje kulala? Amka ukamwite mungu
wako! Huenda akatuangalia, tusiangamie."
7 [g]Kisha mabaharia wakasemezana wao
kwa wao, "Njooni, tupige kura tumtafute
anayehusika na maafa haya." Wakapiga
kura, kura ikamwangukia Yona.
8 [h]Kwa hiyo walimuuliza, "Tuambie, ni
nani anayehusika kwa kutuletea tatizo hili
lote? Unafanya kazi gani? Umetoka wapi?
Nchi yako ni ipi? Wewe ni kutoka taifa
lipi?"
9 [i]Akajibu, "Mimi ni Mwebrania, nami
namwabudu Bwana, Mungu wa Mbinguni,
aliyeumba bahari na nchi kavu."
10 Hili liliwaogopesha nao wakamuuliza,
"Umefanya nini?" (Walijua alikuwa
anamkimbia Bwana, kwa sababu
alishawaambia hivyo.)
11 Bahari ilikuwa inazidi kuchafuka.
Kwa hiyo walimuuliza, "Tukutendee nini
ili kufanya bahari itulie kwa ajili yetu?"
12 [j]Akawajibu, "Niinueni mnitupe
baharini, nayo itakuwa shwari. Ninajua
mawimbi haya makubwa yamewatokea
kwa ajili ya kosa langu."
13 [k]Badala yake, wale watu walijitahidi
kupiga makasia wawezavyo ili wapate
kurudi pwani. Lakini hawakuweza, kwa
kuwa bahari ilizidi kuchafuka kuliko
mwanzo. 14 [l]Ndipo wakamlilia Bwana,
"Ee Bwana, tafadhali usituue kwa
kuondoa uhai wa mtu huyu. Usituhesabie
hatia kwa kuutoa uhai wa mtu asiyekuwa
na hatia, kwa kuwa wewe, Ee Bwana,
umefanya kama ilivyokupendeza." 15 [m]Kisha
walimchukua Yona, wakamtupa baharini
nayo bahari iliyokuwa imechafuka ikatulia.
16 [n]Katika jambo hili watu wakamwogopa
Bwana sana, wakamtolea Bwana dhabihu
na kumwekea nadhiri.
17 [o]Lakini Bwana akamwandaa
nyangumi[p] kummeza Yona, naye Yona
alikuwa ndani ya tumbo la nyangumi kwa
siku tatu, usiku na mchana.

*Maombi Ya Yona Katika Tumbo La Nyangumi*

2 Akiwa ndani ya tumbo la nyangumi,
Yona alimwomba Bwana Mungu wake.
2 [q]Akasema:

[a]**1:1** Mt 16:4; 12:39-41; 2Fal 14:25; Lk 11:29-32
[b]**1:2** Mwa 10:11; 18:20; Yon 3:3; Nah 2:8; Mt 12:41; Ezr 9:6; Yak 5:4
[c]**1:3** Za 139:7; Yos 19:46; Mdo 9:36-43; Mwa 4:16; 10:4; Kut 4:13; Isa 23:1; Yer 20:9
[d]**1:4** Za 107:23-26
[e]**1:5** Mdo 27:18-19
[f]**1:6** Yon 3:8; Mt 8:25; Za 78:34; 107:28
[g]**1:7** Yos 7:10-18; Hes 32:23; Mit 16:33; Mdo 1:26; 1Sam 10:20; 14:43
[h]**1:8** Yos 7:19
[i]**1:9** Dan 2:18; Mdo 17:24; Za 146:6; 96:9; Neh 9:6
[j]**1:12** Mhu 9:18; 2Sam 24:17; 1Nya 21:17
[k]**1:13** Mit 21:30
[l]**1:14** Kum 21:8; Za 115:3; Dan 4:35
[m]**1:15** Za 107:29; Lk 8:24
[n]**1:16** Mk 4:41; Hes 30:2; Za 66:13-14
[o]**1:17** Mt 12:40; 16:4; Lk 11:30; Yn 4:6-7
[p]17 Yaani samaki mkubwa sana.
[q]**2:2** Za 18:6; 120:1; 86:13; Mao 3:55

"Katika shida yangu nalimwita
BWANA,
naye akanijibu.
Kutoka kina cha kaburi[a] niliomba
msaada,
nawe ukasikiliza kilio changu.
3 [b]Ulinitupa kwenye kilindi,
ndani kabisa ya moyo wa bahari,
mikondo ya maji ilinizunguka,
mawimbi yako yote na viwimbi
vilipita juu yangu.
4 [c]Nikasema, 'Nimefukuziwa
mbali na uso wako,
hata hivyo nitatazama tena
kuelekea Hekalu lako takatifu.'
5 [d]Maji yaliyonimeza yalinitisha,
kilindi kilinizunguka;
mwani[e] ulijisokota kichwani
pangu.
6 [f]Nilizama chini sana mpaka pande za
mwisho za milima,
makomeo ya hiyo nchi
yalinifungia hata milele.
Lakini uliuleta uhai wangu kutoka
shimoni,
Ee BWANA Mungu wangu.

7 [g]"Wakati uhai wangu ulipokuwa
unatoka,
nilikukumbuka wewe, BWANA,
nayo maombi yangu yalikufikia
wewe,
katika Hekalu lako takatifu.

8 [h]"Wale watu wanaong'ang'ana na
sanamu zisizofaa
hupoteza neema ile ambayo
ingekuwa yao.
9 [i]Lakini mimi, kwa wimbo wa
shukrani,
nitakutolea dhabihu.
Lile nililowekea nadhiri nitalitimiza.
Wokovu watoka kwa BWANA."

10 [j]Basi BWANA akamwamuru yule nyangumi, naye akamtapika Yona katika nchi kavu.

*Yona Aenda Ninawi*

3 [k]Ndipo neno la BWANA likamjia Yona
mara ya pili: 2 "Ondoka uende katika mji
mkubwa wa Ninawi, ukautangazie ujumbe
ninaokupa."
3 Yona akalitii neno la BWANA naye
akaenda Ninawi. Basi Ninawi ulikuwa
mji maarufu sana, ilichukua siku tatu
kuuzunguka. 4 [lm]Siku ya kwanza, Yona
aliingia mjini. Akatangaza: "Baada ya
siku arobaini Ninawi utaangamizwa."
5 [n]Watu wa Ninawi wakamwamini Mungu,
wakatangaza kufunga, watu wote kuanzia
mkubwa sana hadi yule mdogo kabisa,
wakavaa nguo za gunia.
6 [o]Habari zilipomfikia mfalme wa
Ninawi, aliondoka kwenye kiti chake cha
enzi, akavua majoho yake ya kifalme,
akajifunika nguo ya gunia kisha akaketi
chini mavumbini. 7 [p]Ndipo akatoa tangazo
katika Ninawi yote:

"Kwa amri ya mfalme na wakuu wake:

"Msiruhusu mtu yeyote au mnyama,
makundi ya ng'ombe au wanyama
wengine wafugwao, kuonja kitu
chochote, msiwaruhusu kula wala
kunywa. 8 [q]Bali wanadamu na wanyama
wafunikwe kwa nguo za gunia. Kila

[a]2 Kaburi hapa maana yake ni Kuzimu, kwa Kiebrania ni Sheol.
[b]**2:3** Za 88:6; 42:7; 2Sam 22:5
[c]**2:4** Za 31:22; Yer 7:15; Isa 49:14; 1Fal 8:38, 48
[d]**2:5** Za 69:1-2
[e]5 Mwani hapa maana yake ni magugu yaotayo kwenye sakafu ya kilindi cha bahari.
[f]**2:6** Ay 28:9; 17:16; 33:18; Za 30:3
[g]**2:7** Za 11:4; 18:6; 77:11-12; 34:6; 130:2; Yer 2:13; 2Nya 30:27
[h]**2:8** 1Sam 12:21; Yer 10:8; 2Fal 17:15; Za 31:6; Kum 32:21
[i]**2:9** Hos 14:2; Ebr 13:15; Hes 30:2; Kut 15:2; Za 50:14; 116:14; 66:13-15; 3:8; 42:4
[j]**2:10** Yn 1:17; Mt 8:9
[k]**3:1** Yon 1:1
[l]**3:4** Yer 18:7-10
[m]**3:4** Kum 18:22
[n]**3:5** Mt 12:41; 11:21; Dan 9:3; Lk 11:32
[o]**3:6** Es 4:1-3; Yer 6:26; Mik 1:10; Ay 2:8-13; Eze 27:30-31; Mao 3:29
[p]**3:7** 2Nya 20:3; Ezr 10:6; Yoe 2:15
[q]**3:8** Za 130:1; Yon 1:6; Isa 1:16; Eze 33:11; Dan 4:27; Yer 25:5; 7:3; Ay 16:17

mmoja afanye hima kumwomba
Mungu. Waziache njia zao mbaya na
udhalimu ulio mikononi mwao. 9 [a]Ni
nani ajuaye? Huenda Mungu akaghairi
kwa huruma yake akaacha hasira yake
kali ili tusiangamie.”

10 [b]Mungu alipoona walivyofanya na jinsi
walivyogeuka kutoka njia zao mbaya, akawa
na huruma wala hakuleta maangamizi juu
yao kama alivyokuwa ameonya.

*Hasira Ya Yona Kwa Ajili Ya Huruma Ya Bwana.*

4 [c]Lakini Yona alichukizwa sana
akakasirika. 2 [d]Akamwomba Bwana,
“Ee Bwana, hili si lile nililolisema
nilipokuwa ningali nyumbani? Hii ndiyo
sababu niliharikisha kukimbilia Tarshishi.
Nikifahamu kuwa wewe ni Mungu mwenye
neema na huruma, si mwepesi wa hasira
na umejaa upendo, ni Mungu ambaye
hughairi katika kupeleka maafa. 3 [e]Sasa, Ee
Bwana, niondolee uhai wangu, kwa kuwa
ni afadhali mimi nife kuliko kuishi.”
4 [f]Lakini Bwana akamjibu, “Je unayo
haki yoyote kukasirika?”
5 Yona akatoka nje akaketi mahali upande
wa mashariki wa mji. Hapo akajitengenezea
kibanda, akaketi kwenye kivuli chake na
kungojea ni nini kitakachotokea katika mji.
6 [g]Ndipo Bwana, Mungu akaweka tayari
mzabibu na kuufanya uote, kumpa Yona
kivuli kilichomfunika kichwa ili kuondoa
taabu yake, naye Yona akafurahi sana kwa
ajili ya ule mzabibu. 7 [h]Lakini kesho yake
asubuhi na mapema Mungu akaamuru buu,
autafune mzabibu huo nao ukanyauka.
8 [i]Wakati jua lilipochomoza, Mungu
akautuma upepo wa hari wa mashariki,
nalo jua likawaka juu ya kichwa cha Yona
mpaka akazimia. Akatamani kufa, naye
akasema, “Ni afadhali mimi nife kuliko
kuishi.”
9 Lakini Mungu alimwambia Yona, “Je,
unayo haki kukasirika kuhusu mzabibu
huo?”
Akasema, “Ndiyo, ninayo haki.
Nimekasirika kiasi cha kufa.”
10 Lakini Bwana akamwambia, “Wewe
unakasirika kwa ajili ya mzabibu huu, nawe
hukuusababisha kuota wala kuutunza.
Uliota usiku mmoja, nao ukafa usiku mmoja.
11 [j]Lakini Ninawi ina zaidi ya watu 120,000
ambao hawawezi kupambanua kulia au
kushoto, pamoja na ng’ombe wengi. Je,
hainipasi kufikiri juu ya mji ule mkubwa?”

[a]**3:9** 2Sam 12:22; Yer 18:8; Yoe 2:14; Za 85:3
[b]**3:10** Amo 7:6; Yer 18:8; Kut 32:14
[c]**4:1** Mt 20:11; 20:15; Lk 15:28
[d]**4:2** Yer 20:7-8; Kum 4:31; Za 103:8; Kut 34:6; 22:27; Hes 14:18; Yoe 2:13
[e]**4:3** Hes 11:15; Ay 7:15; Yer 8:3; 1Fal 19:4
[f]**4:4** Mwa 4:6; Mt 20:11-15
[g]**4:6** Yon 1:17
[h]**4:7** Yoe 1:12
[i]**4:8** Za 121:6; 1Fal 19:4
[j]**4:11** Eze 33:11; Kum 1:39; Za 36:6; Yon 1:2; 3:2; 3:1

# MIKA

1 [a]Neno la Bwana lilimjia Mika, Mmoreshethi, wakati wa utawala wa Yothamu, Ahazi na Hezekia, wafalme wa Yuda; ufunuo aliouona kuhusu Samaria na Yerusalemu.

2 [b]Sikieni, enyi mataifa, enyi nyote,
sikilizeni, ee dunia na wote
mliomo ndani yake,
ili Bwana Mwenyezi ashuhudie
dhidi yenu,
Bwana kutoka Hekalu lake
takatifu.

*Hukumu Dhidi Ya Samaria Na Yerusalemu*

3 [c]Tazama! Bwana anakuja kutoka
mahali pake;
anashuka na kukanyaga
mahali palipoinuka juu pa dunia.
4 [d]Milima inayeyuka chini yake
na mabonde yanagawanyika
kama nta mbele ya moto,
kama maji yatiririkayo kasi
kwenye mteremko.
5 [e]Yote haya ni kwa sababu ya kosa la
Yakobo,
ni kwa sababu ya dhambi za
nyumba ya Israeli.
Kosa la Yakobo ni lipi?
Je, sio Samaria?
Je, mahali pa juu pa Yuda pa
kuabudia miungu ni nini?
Je, sio Yerusalemu?

6 [f]"Kwa hiyo nitaufanya Samaria kuwa
lundo la kokoto,
mahali pa kuotesha mizabibu.
Nitayamwaga mawe yake katika
bonde
na kuacha wazi misingi yake.
7 [g]Sanamu zake zote
zitavunjwa vipande vipande;
zawadi zake zote za Hekalu
zitachomwa kwa moto;
nitaharibu vinyago vyake vyote.
Kwa kuwa alikusanya zawadi zake
kutokana na ujira wa kahaba,
nazo zitatumika tena
kulipa mishahara ya kahaba."

*Kulia Na Kuomboleza*

8 [h]Kwa ajili ya hili nitalia na
kuomboleza;
nitatembea bila viatu na tena uchi.
Nitabweka kama mbweha
na kuomboleza kama bundi.
9 [i]Kwa sababu jeraha lake halitibiki;
limekuja Yuda.
Limefika hasa kwenye lango la watu
wangu,
hata Yerusalemu kwenyewe.
10 Usiliseme hili huko Gathi;
usilie hata kidogo.
Huko Beth-le-Afra
gaagaa mavumbini.
11 [j]Piteni mkiwa uchi na wenye aibu,
ninyi mkaao Shafiri.
Wale waishio Saanani
hawatatoka nje.
Beth-Eseli iko katika maombolezo;
kinga yake imeondolewa kwako.
12 [k]Wale waishio Marothi wanagaagaa
kwa maumivu
wakingoja msaada,
kwa sababu maangamizi yamekuja
kutoka kwa Bwana,
hata katika lango la Yerusalemu.

---

[a]**1:1** Yer 26:18; 2Pet 1:21; 1Nya 3:12-13; Hos 1:1; Isa 1:1
[b]**1:2** Kum 4:26; 32:1; Yer 6:19; Mwa 31:50; Za 11:4; Isa 1:2
[c]**1:3** Isa 18:4; 64:1; 26:21; Eze 3:12; Ebr 12:18, 19; Amo 4:13
[d]**1:4** Za 46:2-6; Hes 16:31; Nah 1:5
[e]**1:5** Amo 8:14; Hos 5:5; Yer 2:18-19
[f]**1:6** Kum 20:6; Amo 5:11
[g]**1:7** Eze 6:6; Kut 32:20; Kum 9:21; 23:17-18
[h]**1:8** Isa 15:3; 20:2
[i]**1:9** Yer 46:11; 10:19; 2Fal 18:13; Isa 3:26
[j]**1:11** Eze 23:29
[k]**1:12** Yer 14:19; 40:2

13 [a]Enyi mkaao Lakishi,
fungeni farasi kwenye magari ya vita.
Mlikuwa chanzo cha dhambi
kwa Binti Sayuni,
kwa kuwa makosa ya Israeli
yalikutwa kwako.
14 [b]Kwa hiyo utaipa Moresheth-Gathi
zawadi za kuagana.
Mji wa Akzibu utaonyesha wazi udanganyifu
kwa wafalme wa Israeli.
15 [c]Nitawaleteeni atakayewashinda
ninyi mnaoishi Maresha.
Yeye aliye utukufu wa Israeli
atakuja Adulamu.
16 [d]Nyoeni nywele zenu katika kuomboleza
kwa ajili ya watoto wenu mnaowafurahia;
jifanyieni upara kama tai,
kwa kuwa watawaacha
na kwenda uhamishoni.

*Mipango Ya Mwanadamu Na Ya Mungu*

2 [e]Ole kwa wale wapangao uovu,
kwa wale wafanyao shauri la hila vitandani mwao!
Kunapopambazuka wanalitimiza
kwa sababu uko katika uwezo wao kutekeleza.
2 [f]Wanatamani mashamba na kuyakamata,
pia nyumba na kuzichukua.
Wanamlaghai mwanaume nyumba yake,
mwanadamu mwenzake urithi wake.

3 [g]Kwa hiyo, Bwana asema:
"Ninapanga maangamizi dhidi ya watu hawa,
ambayo hamwezi kujiokoa wenyewe.
Hamtatembea tena kwa majivuno,
kwa kuwa utakuwa ni wakati wa maafa.
4 [h]Siku hiyo watu watawadhihaki,
watawafanyia mzaha
kwa wimbo huu wa maombolezo:
'Tumeangamizwa kabisa;
mali ya watu wangu imegawanywa.
Ameninyang'anya!
Ametoa mashamba yetu kwa wasaliti.' "

5 [i]Kwa hiyo hutakuwa na yeyote katika kusanyiko la Bwana
wa kugawanya mashamba kwa kura.

*Manabii Wa Uongo*

6 [j]Manabii wao husema, "Usitabiri.
Usitabiri kuhusu vitu hivi;
aibu haitatupata."
7 [k]Je, ingesemwa, ee nyumba ya Yakobo:
"Je, Roho wa Bwana amekasirika?
Je, yeye hufanya vitu kama hivyo?"

"Je, maneno yangu hayamfanyii mema
yeye ambaye njia zake ni nyofu?
8 Siku hizi watu wangu wameinuka
kama adui.
Unawavua joho la kitajiri wale wanaopita
pasipo kujali,
kama watu warudio kutoka vitani.

[a]**1:13** Yos 10:3; Za 9:14
[b]**1:14** 2Fal 16:8; Yos 15:44; Yer 15:18
[c]**1:15** Yos 15:44; 12:15
[d]**1:16** Law 13:40; Ay 1:20; 2Fal 18:13; Amo 5:27; Kum 4:27
[e]**2:1** Isa 29:20; 32:7; Es 3:8, 9; Za 36:4; 7:11-14; Hos 7:6; Mwa 31:29
[f]**2:2** Isa 1:23; 5:8; Mit 30:14; Yer 22:17; 1Sam 8:14; Eze 46:18
[g]**2:3** Yer 18:11; 8:3; Amo 3:1-2; Isa 2:12
[h]**2:4** Law 26:31; Yer 4:13; 6:12
[i]**2:5** Kum 32:8, 9, 13; Yos 18:4; Hes 34:13
[j]**2:6** Za 44:13; Yer 19:8; 18:16; 25:18; 29:18; Mik 6:16; Amo 2:12
[k]**2:7** Za 119:65; 15:2; 84:11

9 [a]Unawahamisha wanawake wa watu wangu
kutoka kwenye nyumba zao za kupendeza.
Unaondoa baraka yangu
kwa watoto wao milele.
10 [b]Inuka, nenda zako!
Kwa maana hapa sio mahali pako pa kupumzikia,
kwa sababu pametiwa unajisi,
pameharibiwa, wala hapatengenezeki tena.
11 [c]Ikiwa mwongo na mdanganyifu atakuja na kusema,
'Nitawatabiria divai na pombe kwa wingi,'
angekuwa ndiye nabii
anayekubalika na watu hawa!

*Ahadi Ya Ukombozi*

12 [d]"Hakika nitawakusanya ninyi nyote, ee Yakobo,
Hakika nitawaleta pamoja mabaki ya Israeli.
Nitawaleta pamoja kama kondoo ndani ya zizi,
kama kundi kwenye malisho yake,
mahali hapa patakuwa na msongamano wa watu.
13 [e]Yeye afunguaye njia atawatangulia;
watapita kwenye lango na kutoka nje.
Mfalme wao atawatangulia,
BWANA atakuwa kiongozi."

*Viongozi Na Manabii Wakemewa*

3 [f]Kisha nikasema,
"Sikilizeni enyi viongozi wa Yakobo,
enyi watawala wa nyumba ya Israeli.
Je, hampaswi kujua hukumu,
2 [g]ninyi mnaochukia mema
na kupenda maovu;
ninyi mnaowachuna watu wangu ngozi
na kuondoa nyama kwenye mifupa yao;
3 [h]ninyi mnaokula nyama ya watu wangu,
mnaowachuna ngozi
na kuvunja mifupa yao vipande vipande;
mnaowakatakata kama nyama
ya kuwekwa kwenye sufuria
na kama nyama
ya kuwekwa kwenye chungu?"

4 [i]Kisha watamlilia BWANA,
lakini hatawajibu.
Wakati huo atawaficha uso wake
kwa sababu ya uovu waliotenda.

5 [j]Hili ndilo asemalo BWANA:

"Kuhusu manabii wanaowapotosha watu wangu,
mtu akiwalisha,
wanatangaza 'amani';
kama hakufanya hivyo,
wanaandaa kupigana vita dhidi yake.
6 [k]Kwa hiyo usiku utawajieni, msiweze kuwa na maono,
na giza, msiweze kubashiri.
Jua litawachwea manabii hao,
nao mchana utakuwa giza kwao.
7 [l]Waonaji wataaibika
na waaguzi watafedheheka.
Wote watafunika nyuso zao
kwa sababu hakuna jibu litokalo kwa Mungu."

---

[a]**2:9** Yer 10:20
[b]**2:10** Kum 12:9; Law 18:25-29; Za 106:38-39; Mao 4:15
[c]**2:11** 2Nya 36:16; Yer 5:31; Law 10:9; Isa 30:10
[d]**2:12** Mik 4:6, 7; 5:7; 7:18; Isa 11:11; Sef 3:19; Neh 1:9
[e]**2:13** Isa 52:12; 60:11
[f]**3:1** Yer 5:5
[g]**3:2** Za 53:4; Eze 22:27
[h]**3:3** Za 14:4; Sef 3:3; Ay 24:14; Eze 11:7; 24:4-5; 34:4
[i]**3:4** Kum 1:45; 31:17; 1Sam 8:18; Yer 11:11; Isa 58:4; Mit 1:28; Ay 15:31; Eze 8:18
[j]**3:5** Isa 3:12; 9:16; 53:6; 56:10; Mt 7:15; Yer 4:10
[k]**3:6** Isa 8:19-22; 29:10; Eze 7:26; 12:24
[l]**3:7** Yer 6:15; Mik 7:16; Isa 44:25; Es 6:12; Za 74:9; Amu 8:11; Law 13:45; Eze 20:3

8 [a]Lakini kuhusu mimi, nimejazwa nguvu,
nimejazwa Roho wa BWANA,
haki na uweza,
kumtangazia Yakobo kosa lake,
na Israeli dhambi yake.
9 [b]Sikieni hili, enyi viongozi wa nyumba ya Yakobo,
enyi watawala wa nyumba ya Israeli,
mnaodharau haki
na kupotosha kila lililo sawa;
10 [c]mnaojenga Sayuni kwa kumwaga damu
na Yerusalemu kwa uovu.
11 [d]Viongozi wake wanahukumu kwa rushwa,
na makuhani wake wanafundisha kwa malipo,
nao manabii wake wanatabiri kwa fedha.
Hata hivyo wanamwegemea BWANA na kusema,
"Je, BWANA si yumo miongoni mwetu?
Hakuna maafa yatakayotupata."
12 [e]Kwa hiyo kwa sababu yenu,
Sayuni italimwa kama shamba,
Yerusalemu itakuwa lundo la kokoto,
na kilima cha Hekalu
kitakuwa kichuguu
kilichofunikwa na vichaka.

*Mlima Wa BWANA*

**(Isaya 2:2-4)**

4 [f]Katika siku za mwisho
mlima wa Hekalu la BWANA utaimarishwa
kama mlima mkuu miongoni mwa milima yote;
utainuliwa juu ya vilima,
na watu wa mataifa watamiminika humo.

2 [g]Mataifa mengi yatakuja na kusema,

"Njooni, twendeni mlimani mwa BWANA,
kwenye nyumba ya Mungu wa Yakobo.
Atatufundisha njia zake,
ili tuweze kuenenda katika mapito yake."
Sheria itatoka Sayuni,
neno la BWANA litatoka Yerusalemu.
3 [h]Atahukumu kati ya mataifa mengi,
na ataamua migogoro ya mataifa yenye nguvu na yaliyo mbali.
Watafua panga zao ziwe majembe,
na mikuki yao kuwa miundu ya kukata matawi.
Taifa halitainua upanga dhidi ya taifa jingine,
wala hawatajifunza vita tena.
4 [i]Kila mtu ataketi chini ya mzabibu wake
na chini ya mtini wake,
wala hakuna mtu atakayewaogopesha,
kwa kuwa BWANA Mwenye Nguvu Zote amesema.
5 [j]Mataifa yote yanaweza kutembea
katika jina la miungu yao;

---

[a]**3:8** 1Kor 2:1, 4; Isa 58:1; 57:12; 61:2
[b]**3:9** Isa 58:1-2; 1:23
[c]**3:10** Yer 22:13, 17; Isa 59:7; Mik 7:2; Hab 2:12; Nah 3:1; Eze 22:27
[d]**3:11** Kut 23:8; Law 19:15; Mal 2:9; Eze 22:12; Mik 7:3; Yer 6:13; 1Tim 1:11; 1Sam 4:5-6; Eze 13:19; 34:2; Isa 1:23; 10:20; 56:11; Yer 6:13; 7:4; Mao 4:13; Hos 4:8, 18
[e]**3:12** 2Fal 25:9; Isa 6:11; Mik 1:6; Za 79:1; Yer 52:13; 22:6; Mao 5:18; Eze 5:14
[f]**4:1** Za 48:1; 86:9; Zek 8:3; Isa 2:2; Dan 2:35; 2:44; Eze 17:22; Yer 3:17; 31:12
[g]**4:2** Yer 31:6; Yn 6:45; Eze 20:40; Zek 2:11; 14:16; Isa 54:13; Za 25:8-9; 119:171
[h]**4:3** Isa 2:4; 11:4; Yoe 3:10; Hos 2:18; Za 72:7; Zek 8:20-22; 9:10; Za 46:9
[i]**4:4** 1Fal 4:25; Law 26:6; Eze 39:26; Isa 1:20; 36:16; Yer 31:10; Zek 3:10
[j]**4:5** 2Fal 17:29; Mdo 14:16; Yos 24:14-15; Isa 26:8; Yer 2:11; Zek 10:12

sisi tutatembea katika jina la BWANA
Mungu wetu milele na milele.

*Mpango Wa BWANA*

6 [a]"Katika siku hiyo," asema BWANA,

"nitawakusanya walemavu;
nitawakusanya walio uhamishoni
na wale niliowahuzunisha.
7 [b]Nitawafanya walemavu kuwa mabaki,
wale waliofukuzwa kuwa taifa lenye nguvu.
BWANA atatawala juu yao katika Mlima Sayuni
kuanzia siku hiyo na hata milele.
8 [c]Lakini kuhusu wewe, ee mnara wa ulinzi wa kundi,
ee ngome ya Binti Sayuni,
milki ya awali itarudishwa kwako,
ufalme utakuja kwa Binti Yerusalemu."

9 [d]Kwa nini sasa unalia kwa nguvu:
kwani huna mfalme?
Je, mshauri wako amekufa, hata maumivu yakukamate
kama ya mwanamke
aliye na utungu wa kuzaa?
10 [e]Gaagaa kwa utungu, ee Binti Sayuni,
kama mwanamke mwenye utungu wa kuzaa,
kwa kuwa sasa ni lazima uuache mji
ukapige kambi uwanjani.
Utakwenda Babeli;
huko utaokolewa.
Huko BWANA atakukomboa
kutoka mikononi mwa adui zako.

11 [f]Lakini sasa mataifa mengi
yamekusanyika dhidi yako.
Wanasema, "Mwache anajisiwe,
macho yetu na yatazame Sayuni kwa furaha!"
12 [g]Lakini hawayajui
mawazo ya BWANA;
hawauelewi mpango wake,
yeye awakusanyaye kama miganda
kwenye sakafu ya kupuria.

13 [h]"Inuka upure, ee Binti Sayuni,
kwa kuwa nitakupa pembe za chuma;
nitakupa kwato za shaba
na utavunja vipande vipande mataifa mengi."

Utatoa mapato yao waliopata kwa udanganyifu kwa BWANA,
utajiri wao kwa Bwana wa dunia yote.

*Mtawala Aliyeahidiwa Kutoka Bethlehemu*

5 [i]Panga majeshi yako, ee mji wa majeshi,
kwa kuwa kuzingirwa kumepangwa dhidi yetu.
Watampiga mtawala wa Israeli
shavuni kwa fimbo.

2 [j]"Lakini wewe, Bethlehemu Efrathi,
ingawa u mdogo miongoni mwa koo za Yuda,
kutoka kwako atatokea kwa ajili yangu
yeye atakayekuwa mtawala katika Israeli,
ambaye asili yake ni kutoka zamani,
kutoka milele."

3 [k]Kwa hiyo Israeli utaachwa mpaka wakati
mwanamke aliye na utungu atakapozaa

[a]**4:6** Yer 31:8; Isa 56:8; Za 147:2; 106:47; Eze 34:13, 16; 37:21; Sef 3:19
[b]**4:7** Yoe 2:32; Mik 2:12; Isa 9:6; Mwa 12:2; Dan 2:44; 7:14; Ufu 11:15; Lk 1:33
[c]**4:8** Isa 1:26; Zek 9:9
[d]**4:9** Yer 8:19; 30:6; 48:41; Mwa 3:16
[e]**4:10** Kum 21:10; 2Fal 20:18; Isa 43:14; 48:20
[f]**4:11** Mao 2:16; Oba 1:12; Mik 7:8
[g]**4:12** Mwa 50:20; Isa 55:8; Rum 11:33-34
[h]**4:13** Isa 21:10; 23:18; 45:1; Ufu 21:24; Dan 2:44
[i]**5:1** Ay 16:10; Mt 27:30; Mao 3:30
[j]**5:2** Yn 7:42; Mwa 35:19; 48:7; 1Sam 13:14; Hes 24:19; 2Sam 6:21; 2Nya 7:18; Za 90:2; 132:6; 102:25; Isa 9:6; Mit 8:22; Yn 1:1; Mt 2:6
[k]**5:3** Yer 7:29

na ndugu zake wengine warudi
kujiunga na Waisraeli.

4 [a]Atasimama na kulichunga kundi
lake
katika nguvu ya BWANA,
katika utukufu wa jina la BWANA
Mungu wake.
Nao wataishi kwa usalama, kwa
kuwa wakati huo
ukuu wake utaenea hadi miisho ya
dunia.
5 [b]Naye atakuwa amani yao.

*Ukombozi Na Uharibifu*

Wakati Mwashuru atakapovamia
nchi yetu
na kupita katika ngome zetu,
tutawainua wachungaji saba dhidi
yake,
hata viongozi wanane wa watu.
6 [c]Wataitawala nchi ya Ashuru kwa
upanga,
nchi ya Nimrodi kwa upanga.
Atatuokoa kutoka kwa Mwashuru
atakapoivamia nchi yetu
na kuingia katika mipaka yetu.

7 [d]Mabaki ya Yakobo yatakuwa
katikati ya mataifa mengi
kama umande kutoka kwa BWANA,
kama manyunyu juu ya majani,
ambayo hayamngoji mtu
wala kukawia kwa mwanadamu.
8 [e]Mabaki ya Yakobo yatakuwa
miongoni mwa mataifa,
katikati ya mataifa mengi,
kama simba miongoni mwa
wanyama wa msituni,
kama mwana simba miongoni
mwa makundi ya kondoo,
ambaye anaumiza vibaya na
kuwararua
kila anapopita katikati yao,
wala hakuna awezaye kuokoa.
9 [f]Mkono wako utainuliwa juu kwa
ushindi juu ya watesi wako,
nao adui zako wote
wataangamizwa.

10 [g]"Katika siku ile," asema BWANA,

"nitaangamiza farasi zenu katikati
yenu
na kubomoa magari yenu ya vita.
11 [h]Nitaiangamiza miji ya nchi yenu
na kuziangusha chini ngome zenu
zote.
12 [i]Nitaangamiza uchawi wenu
na hamtapiga tena ramli.
13 [j]Nitaangamiza vinyago vyenu vya
kuchonga
na mawe yenu ya ibada yatoke
katikati yenu;
hamtasujudia tena
kazi ya mikono yenu.
14 [k]Nitang'oa nguzo za Ashera katikati
yenu
na kubomoa miji yenu.
15 [l]Nitalipiza kisasi kwa hasira na
ghadhabu
juu ya mataifa ambayo
hayajanitii."

*Shauri La BWANA Dhidi Ya Israeli*

6 [m]Sikiliza asemalo BWANA:

"Simama, tetea shauri
lako mbele ya milima;
vilima na visikie lile unalotaka
kusema.

[a]**5:4** Isa 40:11; 49:9; 52:13; Za 72:8; Zek 9:10; Mik 7:14; Eze 34:11-15; Lk 1:32
[b]**5:5** Isa 8:7; 9:6; 10:24-27; Lk 2:14; Efe 2:14; Kol 1:19-20
[c]**5:6** Mwa 10:8; Sef 2:13; Lk 1:71; Nah 2:11-13
[d]**5:7** Amo 5:15; Mik 2:12; Isa 44:4; Za 110:3; 133:3
[e]**5:8** Mwa 49:9; Mik 4:13; Zek 10:5; Isa 5:29; Za 50:22; Hos 5:14
[f]**5:9** Za 10:12
[g]**5:10** Kut 15:4, 19; Hos 14:3; Hag 2:22; Zek 9:10
[h]**5:11** Kum 29:23; Isa 6:11; Mao 2:2; Hos 10:14; Amo 5:9
[i]**5:12** Kum 18:10-12; Isa 8:19; 2:9
[j]**5:13** Nah 1:14; Hos 2:10; Isa 2:8; 2:18; Eze 6:9; Zek 13:2
[k]**5:14** Kut 34:13; Amu 3:7; 2Fal 17:10
[l]**5:15** Isa 65:12
[m]**6:1** Za 50:1; Eze 6:2

2 [a]Sikilizeni, ee milima, mashtaka ya BWANA,
sikilizeni, enyi misingi ya milele ya dunia.
Kwa kuwa BWANA ana shauri dhidi ya watu wake;
anatoa mashtaka dhidi ya Israeli.

3 [b]“Watu wangu, nimewatendea nini?
Nimewalemea kwa jinsi gani? Mnijibu.
4 [c]Nimewatoa kutoka Misri na kuwakomboa
kutoka nchi ya utumwa.
Nilimtuma Mose awaongoze,
pia Aroni na Miriamu.
5 [d]Watu wangu, kumbukeni jinsi Balaki mfalme wa Moabu
alivyofanya shauri
na kile Balaamu mwana wa Beori alichojibu.
Kumbukeni safari yenu kutoka Shitimu mpaka Gilgali,
ili mfahamu matendo ya haki ya BWANA.”

6 [e]Nimjie BWANA na kitu gani na kusujudu
mbele za Mungu aliyetukuka?
Je, nije mbele zake na sadaka za kuteketezwa,
nije na ndama za mwaka mmoja?
7 [f]Je, BWANA atafurahishwa na kondoo dume elfu,
au mito elfu kumi ya mafuta?
Je, nimtoe mzaliwa wangu wa kwanza kwa ajili ya kosa langu,
mtoto wangu mwenyewe
kwa ajili ya dhambi ya nafsi yangu?
8 [g]Amekuonyesha yaliyo mema, ee mwanadamu.
BWANA anataka nini kwako?
Ila kutenda kwa haki na kupenda rehema,
na kwenda kwa unyenyekevu na Mungu wako.

*Hatia Na Adhabu Ya Israeli*

9 [h]Sikiliza! BWANA anauita mji:
kulicha jina lako ni hekima:
“Tii hiyo fimbo na yeye aliyeiamuru.
10 [i]Je, bado nisahau, ee nyumba ya uovu,
hazina yako uliyopata kwa udanganyifu
na vipimo vilivyopunguka,
ambavyo vimelaaniwa?
11 [j]Je, naweza kuhukumu kuwa
mtu mwenye mizani ya udanganyifu hana hatia,
aliye na mfuko wa mawe ya kupimia ya uongo?
12 [k]Matajiri wake ni wajeuri;
watu wake ni waongo
na ndimi zao zinazungumza
kwa udanganyifu.
13 Kwa hiyo, nimeanza kukuharibu,
kuwaangamiza kwa sababu ya dhambi zenu.
14 [l]Mtakula lakini hamtashiba;
matumbo yenu bado yatakuwa matupu.
Mtaweka akiba lakini hamtaokoa chochote,
kwa sababu mtakachoweka akiba
nitatoa kwa upanga.

[a]**6:2** Kum 32:1; Hos 12:2; Isa 3:13; Za 50:7; Yer 9:7
[b]**6:3** Za 50:7; Isa 5:3, 4; Yer 2:31; 2:5
[c]**6:4** Kum 7:8; Kut 3:10; 6:6; 4:16; 15:20; Hes 33:1; Za 77:20
[d]**6:5** Hes 22:2-6
[e]**6:6** Yn 6:28; Za 15:1; 40:6-8; 95:2; 51:16-17
[f]**6:7** Isa 1:11; 40:16; Law 18:21; Za 50:8-10; 2Fal 3:27; 16:3; Amo 5:22; Hos 5:6
[g]**6:8** Isa 1:17; Yer 22:3; 23:23; 2Fal 22:19; Isa 57:15; Mwa 5:22; 1Sam 15:22; Kum 10:12-13; Zek 7:9-10; Mt 9:13; Mk 12:33; Lk 11:42
[h]**6:9** Mwa 17:1; Isa 11:4
[i]**6:10** Eze 45:9-10; Amo 3:10; 8:4-6
[j]**6:11** Law 19:36; Hos 12:7; Amu 3:10; Kum 25:13
[k]**6:12** Isa 1:23; 3:8; Za 35:20; 116:11; Yer 9:5
[l]**6:14** Isa 9:20; 30:6; Hos 4:10

15 [a]Mtapanda lakini hamtavuna;
mtakamua zeituni lakini
hamtatumia mafuta yake.
Mtakamua zabibu
lakini hamtakunywa hiyo divai.
16 [b]Mmezishika sheria za Omri
na matendo yote ya nyumba ya
Ahabu,
tena umefuata desturi zao.
Kwa hiyo nitakutoa kwa maangamizi
na watu wako kuwa dhihaka;
mtachukua dharau za mataifa."

*Taabu Ya Israeli*

7 [c]Taabu gani hii niliyo nayo!
Nimefanana na yule
akusanyaye
matunda ya kiangazi,
aokotaye masazo baada ya kuvunwa
shamba la mizabibu;
hakuna kishada chenye matunda ya
kula,
hakuna hata ile tini ya mwanzoni
ninayoitamani.
2 [d]Wanaomcha Mungu wameondolewa
kutoka nchi;
hakuna mtu mnyofu hata mmoja
aliyebaki.
Watu wote wanavizia kumwaga
damu,
kila mmoja anamwinda ndugu
yake kwa wavu.
3 [e]Mikono yote miwili ni hodari katika
kufanya ubaya,
mtawala anadai zawadi,
hakimu anapokea rushwa,
wenye nguvu wanaamuru
wanachotaka:
wote wanafanya shauri baya
pamoja.
4 [f]Aliye mwema kupita wote kati yao
ni kama mchongoma,
anayeonekana mnyofu zaidi
miongoni mwao
ni mbaya kuliko uzio wa miiba.
Siku ya walinzi wako imewadia,
siku atakayokutembelea Mungu.
Sasa ni wakati wao
wa kuchanganyikiwa.
5 Usimtumaini jirani;
usiweke matumaini kwa rafiki.
Hata kwa yule alalaye kifuani
mwako
uwe mwangalifu kwa maneno
yako.
6 [g]Kwa kuwa mwana humdharau baba
yake,
naye binti huinuka dhidi ya mama
yake,
mkwe kuwa kinyume na mama
mkwe wake:
adui wa mtu ni wale wa nyumbani
mwake hasa.

7 [h]Lakini mimi, namtazama Bwana
kwa matumaini,
namngoja Mungu Mwokozi
wangu;
Mungu wangu atanisikia mimi.

*Israeli Atainuka*

8 [i]Usifurahie msiba wangu, ee adui
yangu!
Ingawa nimeanguka, nitainuka.
Japo ninaketi gizani,
Bwana atakuwa nuru yangu.
9 [j]Kwa sababu nimetenda dhambi
dhidi yake,
nitabeba ghadhabu ya Bwana,
mpaka atakaponitetea shauri langu
na kuithibitisha haki yangu.

---

[a]**6:15** Kum 28:36-38; Yer 12:13; Ay 24:11; Amo 5:11; Sef 1:13
[b]**6:16** 1Fal 16:25, 29-33; Yer 7:24; 25:9; 51:51; Mik 2:6
[c]**7:1** Yer 2:3; Hos 9:10; Wim 2:13
[d]**7:2** Za 10:8; 12:1; 57:6; Yer 2:29; 8:6; 5:26; Mit 6:17; 1Sam 24:11; Hab 1:15; Mik 3:10; Isa 3:5
[e]**7:3** Mit 4:16; Kut 23:8; Hos 4:18; Isa 1:23; Eze 22:12
[f]**7:4** Hes 33:55; Eze 2:6; Ay 31:14; 2Sam 23:6; Isa 22:5; Hos 9:7
[g]**7:6** Eze 22:7; Mwa 9:22-24; Mt 10:21, 35-36; Mk 13:12
[h]**7:7** Isa 21:8; 25:9; Za 4:3; 130:5
[i]**7:8** Za 20:8; 22:17; 37:24; 37:5, 6; Mit 24:17; Mik 4:11; Mao 4:21; 2Sam 22:29; Isa 9:2
[j]**7:9** Mao 3:39-40; Za 107:10; 119:154; Isa 46:13

Atanileta nje kwenye mwanga,
nami nitaiona haki yake.
10 [a]Kisha adui yangu ataliona
naye atafunikwa na aibu,
yule aliyeniambia,
“Yu wapi BWANA Mungu wako?”
Macho yangu yataona kuanguka kwake,
hata sasa atakanyagwa chini ya mguu
kama tope barabarani.

11 [b]Siku ya kujenga kuta zako itawadia,
siku ya kupanua mipaka yako.
12 [c]Siku hiyo watu watakuja kwako
kutoka Ashuru na miji ya Misri,
hata kutoka Misri hadi Frati
na kutoka bahari hadi bahari
na kutoka mlima hadi mlima.
13 [d]Dunia itakuwa ukiwa kwa sababu ya wakazi wake,
kwa sababu ya matunda ya matendo yao.

*Sala Na Sifa*

14 [e]Wachunge watu wako kwa fimbo yako,
kundi la urithi wako,
ambalo linaishi peke yake msituni,
katika nchi ya malisho yenye rutuba.
Waache walishe katika Bashani na Gileadi
kama ilivyokuwa siku za kale.

15 [f]“Kama siku zile mlipotoka Misri,
nitawaonyesha maajabu yangu.”

16 [g]Mataifa yataona na kuaibika,
waliondolewa nguvu zao zote.
Wataweka mikono yao kwenye vinywa vyao
na masikio yao yatakuwa na uziwi.
17 [h]Wataramba mavumbi kama nyoka,
kama viumbe vitambaavyo juu ya ardhi.
Watatoka nje ya mapango yao wakitetemeka;
watamgeukia BWANA Mungu wetu kwa hofu
nao watakuogopa.
18 [i]Ni nani Mungu kama wewe,
ambaye anaachilia dhambi
na kusamehe makosa
ya mabaki ya urithi wake?
Wewe huwi na hasira milele,
bali unafurahia kuonyesha rehema.
19 [j]Utatuhurumia tena,
utazikanyaga dhambi zetu
chini ya nyayo zako,
na kutupa maovu yetu yote
katika vilindi vya bahari.
20 [k]Utakuwa wa kweli kwa Yakobo,
nawe utamwonyesha Abrahamu rehema,
kama ulivyowaahidi kwa kiapo baba zetu
siku za kale.

---

[a]**7:10** Za 35:26; 42:3; Isa 5:5; 51:23; Ay 40:12; Zek 10:5; 2Sam 22:43
[b]**7:11** Amo 9:11; Isa 54:11
[c]**7:12** Isa 19:23-25; 11:11; 60:4
[d]**7:13** Isa 3:10-11; Eze 12:19; 33:28-29
[e]**7:14** Za 23:4; 28:9; 95:7; Mik 5:4; 7:14; Hes 23:9; Kum 33:28; Wim 4:1; Isa 33:9; Yer 50:19; Eze 36:11
[f]**7:15** Kut 3:20; Za 78:12
[g]**7:16** Isa 26:11; Amu 18:19
[h]**7:17** Mwa 3:14; 2Sam 22:46; Isa 25:3; 59:19
[i]**7:18** Kut 10:8; 1Sam 2:2; Isa 43:25; 54:9; 57:16; Zek 3:4; Yer 31:20; 50:20; Kut 15:11; 34:6, 7, 9; Za 89:6-8; 103:9; 2Nya 6:21; 30:9; Za 103:8-13; Yoe 2:32; Amo 5:15; Mik 2:12
[j]**7:19** Isa 43:25; Rum 6:6; Yer 31:34
[k]**7:20** Gal 3:16; Kum 11:29; 7:8; Lk 1:72; Za 108:4

# NAHUMU

1 [a]Neno alilosema Mungu kuhusu Ninawi. Kitabu cha maono cha Nahumu, Mwelkoshi.

*Hasira Ya Mungu Dhidi Ya Ninawi*

2 [b]BWANA ni mwenye wivu na Mungu
mlipiza kisasi;
BWANA hulipiza kisasi na amejaa
ghadhabu.
BWANA hulipiza kisasi juu ya watesi
wake,
naye anadumisha ghadhabu yake
dhidi ya adui zake.
3 [c]BWANA si mwepesi wa hasira naye
ni mwenye nguvu,
BWANA hataacha kuadhibu wenye
hatia.
Njia yake ipo katika kisulisuli na
tufani,
na mawingu ni vumbi la miguu
yake.
4 [d]Anakemea bahari na kuikausha,
anafanya mito yote kukauka.
Bashani na Karmeli zinanyauka
na maua ya Lebanoni hukauka.
5 [e]Milima hutikisika mbele yake
na vilima huyeyuka.
Nchi hutetemeka mbele yake,
dunia na wote waishio ndani yake.
6 [f]Ni nani awezaye kuzuia hasira yake
yenye uchungu?
Nani awezaye kuvumilia hasira
yake kali?
Ghadhabu yake imemiminwa kama
moto,
na miamba inapasuka mbele zake.
7 [g]BWANA ni Mwema,
kimbilio wakati wa taabu.
Huwatunza wale wanaomtegemea,
8 [h]lakini kwa mafuriko makubwa,
ataangamiza Ninawi;
atafuatilia adui zake hadi gizani.

9 [i]Shauri baya lolote wapangalo dhidi
ya BWANA
yeye atalikomesha;
taabu haitatokea mara ya pili.
10 [j]Watasongwa katikati ya miiba
na kulewa kwa mvinyo wao.
Watateketezwa kama mabua
makavu.
11 Ee Ninawi, kutoka kwako
amejitokeza mmoja,
ambaye anapanga shauri baya
dhidi ya BWANA
na kushauri uovu.

12 [k]Hili ndilo asemalo BWANA:

"Ingawa wana muungano nao ni
wengi sana,
watakatiliwa mbali na kuangamia.
Ingawa nimekutesa wewe, ee Yuda,
sitakutesa tena.
13 [l]Sasa nitavunja nira zao kutoka
shingo yako,
nami nitazivunjilia mbali pingu
zako."

14 [m]Hii ndiyo amri BWANA aliyoitoa
kukuhusu wewe, Ninawi:
"Hutakuwa na wazao
watakaoendeleza jina lako.
Nitaharibu sanamu za kuchonga na
sanamu za kuyeyusha
ambazo zipo katika hekalu la
miungu yenu.

[a]**1:1** Isa 13:1; 19:1; Yer 23:33-34; 50:18; Mwa 10:11; Nah 2:8; 3:7
[b]**1:2** Kut 20:5; Mwa 4:24; Kum 32:41; 7:10; Za 94:1
[c]**1:3** Neh 9:17; Kut 34:7; 19:16; Za 103:8; Mik 7:18; 2Sam 22:10; Za 50:3; 104:3
[d]**1:4** 2Sam 22:16; Kut 14:22; Isa 33:9; Yos 3:15, 16
[e]**1:5** Kut 19:18; Ay 9:6; 2Sam 22:8; Yoe 2:10; Eze 38:20; Mik 1:4
[f]**1:6** Za 130:3; Eze 22:14; Isa 5:24-25; 42:25; Yer 10:10; 1Fal 19:11
[g]**1:7** Yer 33:11; 17:17; Za 22:9; 1:6; 2Tim 2:19
[h]**1:8** Isa 8:7; Amo 8:8; Dan 9:26
[i]**1:9** Hos 7:15
[j]**1:10** 2Sam 23:6; Isa 49:26; 5:24; Mal 4:1
[k]**1:12** Isa 10:34; 54:6-8; Mao 3:31-32
[l]**1:13** Isa 9:4; Ay 12:18; Za 107:14
[m]**1:14** Isa 14:22; Mik 5:13; Yer 28:8; Eze 32:22-23

Nitaandaa kaburi lako,
kwa maana wewe ni mwovu
kabisa."

15 [a]Tazama, huko juu milimani,
miguu ya huyo mmoja aletaye
habari njema,
ambaye anatangaza amani!
Ee Yuda, sherehekea sikukuu zako,
nawe utimize nadhiri zako.
Waovu hawatakuvamia tena;
wataangamizwa kabisa.

*Ninawi Kuanguka*

2 [b]Mshambuliaji anasogea dhidi yako,
Ninawi.
Linda ngome,
chunga barabara,
jitieni nguvu wenyewe,
kusanya nguvu zako zote!
2 [c]BWANA atarudisha fahari ya
Yakobo,
kama fahari ya Israeli,
ingawa waangamizi wamewaacha
ukiwa
na wameharibu mizabibu yao.

3 [d]Ngao za askari wake ni nyekundu,
mashujaa wamevaa nguo
nyekundu.
Chuma kwenye magari ya vita
chametameta,
katika siku aliyoyaweka tayari,
mikuki ya mierezi inametameta.
4 [e]Magari ya vita yanafanya
msukosuko barabarani,
yakikimbia nyuma na mbele
uwanjani.
Yanaonekana kama mienge ya moto;
yanakwenda kasi kama umeme.

5 [f]Anaita vikosi vilivyochaguliwa,
lakini bado wanajikwaa njiani.
Wanakimbilia haraka kwenye ukuta
wa mji,
ile ngao ya kuwakinga
imetayarishwa.
6 [g]Malango ya mto yamefunguliwa
wazi,
na jumba la kifalme limeanguka.
7 [h]Imeagizwa kwamba mji uchukuliwe
na upelekwe uhamishoni.
Vijakazi wake wanaomboleza kama
hua
na kupigapiga vifua vyao.
8 Ninawi ni kama dimbwi,
nayo maji yake yanakauka.
Wanalia, "Simama! Simama!"
Lakini hakuna anayegeuka nyuma.
9 Chukueni nyara za fedha!
Chukueni nyara za dhahabu!
Wingi wake hauna mwisho,
utajiri kutoka hazina zake zote!
10 [i]Ameharibiwa, ametekwa nyara,
ameachwa uchi!
Mioyo inayeyuka, magoti
yanalegea,
miili inatetemeka,
na kila uso umebadilika rangi.

11 [j]Liko wapi sasa pango la simba,
mahali ambapo waliwalisha
watoto wao,
ambapo simba dume na simba jike
walikwenda
na ambapo wana simba
walikwenda
bila kuogopa chochote?
12 [k]Simba aliua mawindo ya kutosha
watoto wake,
alinyonga mawindo kwa ajili ya
mwenzi wake,
akijaza makao yake kwa alivyoua
na mapango yake kwa mawindo.

---

[a]**1:15** Isa 40:9; Rum 10:15; Isa 52:7; Mdo 10:36; Law 23:2-4
[b]**2:1** Yer 51:20
[c]**2:2** Eze 37:23; Isa 60:15
[d]**2:3** Eze 23:14-15
[e]**2:4** Yer 4:13; Eze 23:24
[f]**2:5** Yer 46:12
[g]**2:6** Isa 45:1; Nah 3:13
[h]**2:7** Mwa 8:8; Isa 59:11; 32:12
[i]**2:10** Yos 2:11; 7:5; Isa 29:22
[j]**2:11** Isa 5:29
[k]**2:12** Yer 51:34; 4:7; Isa 37:18

13 [a]Bwana Mwenye Nguvu Zote
anatangaza,
"Mimi ni kinyume na ninyi.
Magari yenu ya vita nitayateketeza
kwa moto,
na upanga utakula wana simba
wako.
Sitawaachia mawindo juu ya nchi.
Sauti za wajumbe wako
hazitasikika tena."

*Ole Wa Ninawi*

3 [b]Ole wa mji umwagao damu,
uliojaa uongo,
umejaa nyara,
usiokosa kuwa na vitu vya kuteka
nyara.
2 [c]Kelele za mijeledi,
vishindo vya magurudumu,
farasi waendao mbio
na mshtuo wa magari ya vita!
3 Wapanda farasi wanaenda mbio,
panga zinameremeta,
na mikuki inang'aa!
Majeruhi wengi,
malundo ya maiti,
idadi kubwa ya miili isiyohesabika,
watu wanajikwaa juu ya mizoga:
4 [d]yote haya kwa sababu ya wingi wa
tamaa za kahaba,
anayeshawishi, bibi wa mambo ya
uchawi,
anayewatia utumwani mataifa kwa
ukahaba wake
na pia jamaa za watu kwa ulozi
wake.

5 [e]Bwana Mwenye Nguvu Zote
anasema,
"Mimi ni kinyume na ninyi.
Nitafunika uso wako kwa gauni
lako.
Nitaonyesha mataifa uchi wako
na falme aibu yako.
6 [f]Nitakutupia uchafu,
nitakufanyia dharau
na kukufanya kioja.
7 [g]Wote wanaokuona watakukimbia na
kusema,
'Ninawi ipo katika kuangamia:
ni nani atakayeomboleza kwa ajili
yake?'
Nitampata wapi yeyote wa
kukufariji?"

8 [h]Je, wewe ni bora kuliko No-Amoni,
uliopo katika Mto Naili,
uliozungukwa na maji?
Mto ulikuwa kinga yake,
nayo maji yalikuwa ukuta wake.
9 [i]Kushi[j] na Misri walikuwa nguvu
zake zisizo na mpaka;
Putu na Libia walikuwa miongoni
mwa wale walioungana naye.
10 [k]Hata hivyo alichukuliwa mateka
na kwenda uhamishoni.
Watoto wake wachanga walivunjwa
vunjwa vipande
kwenye mwanzo wa kila barabara.
Kura zilipigwa kwa watu wake
wenye heshima,
na watu wake wote wakuu
walifungwa kwa minyororo.
11 [l]Wewe pia utalewa;
utakwenda mafichoni
na kutafuta kimbilio kutoka kwa
adui.

12 [m]Ngome zako zote ni kama mitini
yenye matunda yake ya kwanza
yaliyoiva;
wakati inapotikiswa,
tini huanguka kwenye kinywa
chake alaye.

[a]**2:13** Isa 10:5-13; Yer 21:13; Nah 3:5; Za 46:9; 2Sam 2:26; Mik 5:6
[b]**3:1** Eze 22:2; Mik 3:10; Za 12:2
[c]**3:2** Isa 34:3; Yer 47:3
[d]**3:4** Isa 47:9; 23:17; 2The 2:9, 10; Dan 2:2; Ufu 9:20, 21; Eze 16:25-29
[e]**3:5** Nah 2:13; Isa 47:2-3; 20:4; Yer 13:22
[f]**3:6** Kut 29:14; Ay 9:31; 1Sam 2:30; Yer 51:37; Isa 14:16
[g]**3:7** Isa 13:14; 31:9; Nah 1:1; Ay 3:14; Yer 51:37
[h]**3:8** Amo 6:2; Yer 46:25; Isa 19:6-9
[i]**3:9** Mwa 10:6; 2Nya 12:3; Eze 27:10; 30:5
[j]9 Kushi ni Ethiopia.
[k]**3:10** Isa 20:4; 2Fal 8:12; Isa 13:16; Hos 13:16; Ay 6:26-27; Eze 24:6; Yer 40:1; Yoe 3:3; Oba 1:11
[l]**3:11** Isa 49:26; 2:10
[m]**3:12** Wim 2:13; Ufu 6:13; Isa 28:4

13 [a]Tazama vikosi vyako:
wote ni wanawake!
Malango ya nchi yako
yamekuwa wazi kwa adui zako;
moto umeteketeza mapingo yake.

14 [b]Teka maji kwa ajili ya kuzingirwa
kwako,
imarisha ulinzi wako,
Ufanyie udongo wa mfinyanzi kazi,
yakanyage matope,
karabati tanuru la kuchomea
matofali!
15 [c]Huko moto utakuteketeza,
huko upanga utakuangusha chini
na kama vile panzi, watakumaliza.
Ongezeka kama panzi,
ongezeka kama nzige!
16 [d]Umeongeza idadi ya
wafanyabiashara wako
mpaka wamekuwa wengi kuliko
nyota za angani,
lakini kama nzige wanaacha nchi
tupu
kisha huruka na kwenda zake.
17 [e]Walinzi wako ni kama nzige,
maafisa wako ni kama makundi ya
nzige
watuao kwenye kuta wakati wa
siku ya baridi:
lakini wakati jua linapotokea
wanaruka kwenda zao,
na hakuna ajuaye waendako.

18 [f]Ee mfalme wa Ashuru, wachungaji
wako wanasinzia;
wakuu wako wanalala chini
mavumbini kupumzika.
Watu wako wametawanyika juu ya
milima
bila kuwa na mtu yeyote wa
kuwakusanya.

19 [g]Hakuna kitu kinachoweza kuponya
jeraha lako;
jeraha lako ni la kukuua.
Kila anayesikia habari zako,
hupiga makofi kwa kuanguka
kwako,
kwa kuwa ni nani ambaye
hajaguswa
na ukatili wako usio na mwisho?

[a]**3:13** Isa 19:16; 45:2; Yer 50:37; Nah 2:6
[b]**3:14** 2Nya 32:4; Nah 2:1
[c]**3:15** Isa 27:1; 2Sam 2:26; Yer 51:14; Yoe 1:4
[d]**3:16** Kut 10:13
[e]**3:17** Ufu 9:7; Yer 51:17
[f]**3:18** Za 76:5-6; Yer 25:27; 50:18; Eze 31:3; Isa 56:10; 1Fal 22:17
[g]**3:19** Yer 30:13; Mik 1:9; Ay 27:23; Mao 2:15; Sef 2:15; Isa 14:8; 37:18

# HABAKUKI

1 [a]Neno alilopokea nabii Habakuki.

*Lalamiko La Habakuki*

2 [b]Ee BWANA, hata lini nitakuomba msaada,
lakini wewe husikilizi?
Au kukulilia, "Udhalimu!"
Lakini hutaki kuokoa?
3 [c]Kwa nini unanifanya nitazame dhuluma?
Kwa nini unavumilia makosa?
Uharibifu na udhalimu viko mbele yangu;
kuna mabishano na mapambano kwa wingi.
4 [d]Kwa hiyo sheria imepotoshwa,
nayo haki haipo kabisa.
Waovu wanawazunguka wenye haki,
kwa hiyo haki imepotoshwa.

*Jibu La BWANA*

5 "Yatazame mataifa,
uangalie na ushangae kabisa.
Kwa sababu katika siku zako nitafanya kitu
ambacho hungeamini,
hata kama ungeambiwa.
6 Nitawainua Wakaldayo,
watu hao wakatili na wenye haraka,
ambao hupita dunia yote
kuteka mahali pa kuishi pasipo pao wenyewe.
7 Ni watu wanoogopwa na wanaotisha;
wenyewe ndio sheria yao,
na huinua heshima yao wenyewe.
8 Farasi wao ni wepesi kuliko chui,
na wakali kuliko mbwa mwitu wakati wa machweo.
Askari wapanda farasi wao huenda mbio;
waendesha farasi wao wanatoka mbali.
Wanaruka kasi kama tai ili kurarua;
9 [e]wote wanakuja tayari kwa fujo.
Makundi yao ya wajeuri yanasonga mbele
kama upepo wa jangwani,
na kukusanya wafungwa
kama mchanga.
10 [f]Wanawabeza wafalme,
na kuwadhihaki watawala.
Wanaicheka miji yote
iliyozungushiwa maboma;
wanafanya malundo ya udongo na kuiteka hiyo miji.
11 [g]Kisha wanapita kasi kama upepo na kusonga mbele:
watu wenye hatia, ambao nguvu zao ndio mungu wao."

*Lalamiko La Pili La Habakuki*

12 [h]Ee BWANA, je, wewe sio wa tangu milele?
Mungu wangu, Uliye Mtakatifu wangu, hatutakufa.
Ee BWANA, umewachagua wao ili watekeleze hukumu;
Ee Mwamba, umewaamuru watuadhibu.
13 [i]Macho yako ni safi mno hata yasiweze kuutazama uovu,
wala huwezi kuvumilia makosa.
Kwa nini basi unawavumilia wadanganyifu?
Kwa nini unakuwa kimya wakati waovu
wanawameza wale wenye haki
kuliko wao wenyewe?

---

[a]**1:1** Nah 1:1
[b]**1:2** Za 13:1-2; 22:1-2; 6:3; 27:7; Yer 14:9
[c]**1:3** Ay 9:23; Yer 20:8; Za 55:9
[d]**1:4** Ay 12:6; Za 12:8; 58:2
[e]**1:9** Hab 2:5
[f]**1:10** 2Nya 36:6; Yer 33:4
[g]**1:11** Yer 4:11-12; Dan 4:30
[h]**1:12** Mwa 21:33; Isa 31:1; 37:23; Kut 33:22; Isa 10:6; Mwa 49:24; Za 118:17
[i]**1:13** Za 18:26; Mao 3:34-36; Za 25:3; Ay 21:7

14 Umewafanya watu kama samaki baharini,
kama viumbe wa bahari wasio na mtawala.
15 [a]Adui mwovu anawavuta wote kwa ndoana,
anawakamata katika wavu wake,
anawakusanya katika juya lake;
kwa hiyo anashangilia na anafurahi.
16 [b]Kwa hiyo anatoa kafara kwa wavu wake,
na kuchoma uvumba kwa juya lake,
kwa kuwa kwa wavu wake anaishi kwa starehe,
na anafurahia chakula kizuri.
17 [c]Je, aendelee kuwatoa walio katika wavu wake,
akiangamiza mataifa bila huruma?

2 1 [d]Nitasimama katika zamu yangu,
na kujiweka mwenyewe juu ya maboma;
nitatazama nione atakaloniambia,
na ni jibu gani nitakalotoa kuhusu lalamiko hili.

*Jibu La Bwana*

2 [e]Kisha BWANA akajibu:

"Andika ufunuo huu,
na ukaufanye wazi juu ya vibao,
ili mpiga mbiu akimbie nao.
3 [f]Kwa kuwa ufunuo huu unasubiri wakati uliokubalika;
unazungumzia mambo ya mwisho,
na kamwe hautakosea.
Iwapo utakawia, wewe usubiri;
kwa hakika utakuja na hautachelewa.

4 [g]"Tazama, amejaa majivuno;
anavyovitamani si vya unyofu:
lakini mwenye haki ataishi kwa imani yake:
5 [h]hakika mvinyo humsaliti;
ni mwenye kiburi na hana amani.
Kwa sababu ni mlafi kama kuzimu
na kama kifo kamwe hatosheki;
anajikusanyia mataifa yote
na kuchukua watu wote mateka.

6 [i]"Je, watu wote hawatamsuta kwa
dhihaka na kumbeza, wakisema,

" 'Ole wake yeye akusanyaye bidhaa zilizoibwa
na kujifanyia utajiri kwa kutoza kwa nguvu!
Ataendelea hivi kwa muda gani?'
7 [j]Je, wadai wako hawatainuka ghafula?
Je, hawataamka na kukufanya utetemeke?
Kisha utakuwa mhanga kwao.
8 [kl]Kwa kuwa umeteka nyara mataifa mengi,
watu waliobaki watakuteka nyara wewe.
Kwa kuwa umemwaga damu ya mtu;
umeharibu nchi na miji, na kila mmoja ndani yake.

9 [m]"Ole wake yeye ajengaye milki yake kwa mapato ya udhalimu,
awekaye kiota chake juu,
ili kukimbia makucha ya uharibifu!
10 [n]Umefanya shauri la maangamizi ya watu wengi,
ukiaibisha nyumba yako

[a]**1:15** Yer 5:26; Isa 19:8; Ay 18:8; Yer 16:16
[b]**1:16** Yer 44:8
[c]**1:17** Isa 14:6; 19:8
[d]**2:1** Isa 21:8; Za 48:13; 85:8; Eze 3:17; Za 73:16, 17; 5:3
[e]**2:2** Isa 8:1; 30:8; Kum 27:8; Rum 4:24; 15:4; Yer 36:2; Eze 24:2; Ufu 1:19
[f]**2:3** Dan 10:14; 11:27; 8:17; Za 27:14; Eze 12:25
[g]**2:4** Eze 18:9; Yn 3:36; 2Kor 5:7; Rum 1:17; Gal 3:11; Ebr 10:37-38
[h]**2:5** Mit 20:1; Isa 2:11; Mit 27:20; 30:15-16; Hab 1:9
[i]**2:6** Isa 14:4; Amo 2:8
[j]**2:7** Mit 29:1
[k]**2:8** Zek 1:12
[l]**2:8** Isa 33:1; Yer 50:17-18; Oba 1:15; Zek 2:8-9; Eze 39:10
[m]**2:9** Yer 22:13; 51:13; Ay 39:27; Isa 10:14
[n]**2:10** Yer 26:19; Nah 3:6

mwenyewe, na kupotewa na
maisha yako.
11 [a]Mawe ya kuta yatapiga kelele,
na mihimili ya kazi ya mbao
itarudisha mwangwi wake.

12 [b]"Ole wake yeye ajengaye mji kwa
kumwaga
damu na kuusimamisha mji kwa
uhalifu!
13 [c]Je, BWANA Mwenye Nguvu Zote
hakuonyesha
kwamba kazi ya wanadamu ni
mafuta tu kwa ajili ya moto,
na kwamba mataifa
yanajichosha bure?
14 [d]Kwa kuwa dunia itajazwa na
maarifa ya utukufu wa
BWANA,
kama maji yaifunikavyo bahari.

15 [e]"Ole wake yeye awapaye jirani zake
kileo,
akiimimina kutoka kwenye kiriba
cha mvinyo mpaka wamelewa,
ili apate kutazama miili yao iliyo
uchi.
16 [f]Utajazwa na aibu badala ya
utukufu.
Sasa ni zamu yako! Kunywa na
ujifunue!
Kikombe kutoka kwenye mkono wa
kuume wa BWANA kinakujia,
na aibu itafunika utukufu wako.
17 [g]Ukatili ulioifanyia Lebanoni
utakufunika,
na uharibifu uliowafanyia
wanyama utakutisha.
Kwa sababu umemwaga damu ya
mtu;
umeharibu nchi na miji na kila
mmoja aliyeko ndani yake.

18 [h]"Sanamu ina thamani gani,
kwani mwanadamu ndiye
alichonga?
Ama kinyago kinachofundisha
uongo?
Kwa kuwa yeye aliyekitengeneza
hutegemea kazi ya mikono yake
mwenyewe;
hutengeneza sanamu zisizoweza
kuzungumza.
19 [i]Ole wake yeye auambiaye mti, 'Uwe
hai!'
Ama asemaye na jiwe lisilo na
uhai, 'Amka!'
Je, linaweza kuongoza?
Limefunikwa kwa dhahabu na
fedha;
hakuna pumzi ndani yake.
20 [j]Lakini BWANA yuko katika Hekalu
lake takatifu;
dunia yote na inyamaze mbele
yake."

*Maombi Ya Habakuki*

3 Sala ya nabii Habakuki iliyoimbwa kwa shigionothi.[k]

2 [l]BWANA, nimezisikia sifa zako;
nami naogopa kwa matendo yako,
Ee BWANA.
Fufua kazi yako katikati ya miaka,
katikati ya miaka tangaza habari
yako;
katika ghadhabu kumbuka
rehema.

3 [m]Mungu alitoka Temani,
yeye Aliye Mtakatifu kutoka
Mlima Parani.
Utukufu wake ulifunika mbingu,
na sifa zake zikaifunika dunia.

---

[a]**2:11** Yos 24:27; Zek 5:4; Lk 19:40
[b]**2:12** Eze 22:2; Mik 3:10
[c]**2:13** Isa 50:11; 47:13
[d]**2:14** Kut 16:7; Hes 14:21; Isa 11:9
[e]**2:15** Mit 23:20
[f]**2:16** Eze 23:32-34; Hos 4:7; Law 10:9; Mao 4:21; Za 16:5; Isa 51:22
[g]**2:17** Yer 50:33; 51:35; 50:15
[h]**2:18** 1Sam 12:21; Amu 10:14; Isa 40:19; Yer 5:21; 14:22; 10:14; 1Kor 12:2
[i]**2:19** 1Fal 18:27; Yer 10:4; Hos 4:12; Dan 5:4, 23
[j]**2:20** Za 11:4; Isa 41:1
[k]1 Ni kifaa cha uimbaji chenye nyuzi; pia maombi kutumia kifaa hiki.
[l]**3:2** Ay 26:14; Za 119:120; 90:16; 44:1; 85:6; Isa 54:8
[m]**3:3** Mwa 36:11, 15; Isa 31:1; Hes 10:12; Za 48:10

4 [a]Mng'ao wake ulikuwa kama jua
lichomozalo;
mionzi ilimulika kutoka mkononi
mwake,
ambako nguvu zake zilifichwa.
5 [b]Tauni ilimtangulia;
maradhi ya kuambukiza yalifuata
nyayo zake.
6 [c]Alisimama, akaitikisa dunia;
alitazama, na kuyafanya mataifa
yatetemeke.
Milima ya zamani iligeuka mavumbi
na vilima vilivyozeeka
vikaanguka.
Njia zake ni za milele.
7 [d]Niliona watu wa Kushani katika
dhiki,
na makazi ya Midiani katika
maumivu makali.

8 [e]Ee BWANA, uliikasirikia mito?
Je, ghadhabu yako ilikuwa dhidi
ya vijito?
Je, ulighadhibikia bahari
ulipoendesha farasi wako
na magari yako ya ushindi?
9 [f]Uliufunua upinde wako
na kuita mishale mingi.
Uliigawa dunia kwa mito;
10 [g]milima ilikuona ikatetemeka.
Mafuriko ya maji yakapita huko;
vilindi vilinguruma
na kuinua mawimbi yake juu.

11 [h]Jua na mwezi vilisimama kimya
mbinguni
katika mng'ao wa mishale yako
inayoruka,
na katika mng'ao wa mkuki wako
umeremetao.
12 [i]Kwa ghadhabu ulipita juu ya dunia,
na katika hasira ulikanyaga
mataifa.
13 [j]Ulikuja kuwaokoa watu wako,
kumwokoa uliyemtia mafuta.
Ulimponda kiongozi wa nchi ya
uovu,
ukamvua toka kichwani hadi
wayo.
14 [k]Kwa mkuki wake mwenyewe
ulitoboa kichwa chake
wakati mashujaa wake
walifurika nje kwa kishindo
kututawanya,
wakifurahi kama walio karibu
kutafuna
wale wanyonge waliokuwa
mafichoni.
15 [l]Ulikanyaga bahari kwa farasi wako,
ukisukasuka maji makuu.

16 [m]Nilisikia na moyo wangu ukagonga
kwa nguvu,
midomo yangu ikatetemeka kwa
hofu niliposikia sauti;
uchakavu ukanyemelea mifupa
yangu,
na miguu yangu ikatetemeka.
Hata hivyo nitasubiri kwa uvumilivu
siku ya maafa
kuyajilia mataifa yaliyotuvamia.
17 [n]Ingawa mtini hauchanui maua
na hakuna zabibu juu ya
mizabibu,
ingawaje mzeituni hauzai,
na hata mashamba hayatoi
chakula,
iwapo hakuna kondoo katika banda,
wala ng'ombe katika zizi,

---

[a]**3:4** Isa 18:4; Ay 9:6
[b]**3:5** Law 26:25
[c]**3:6** Za 46:2; 114:1-6; 18:7; Kut 19:18; 23:31; Kum 32:8; Hes 21:24, 34; Mwa 49:26; 21:33
[d]**3:7** Mwa 25:2; Hes 25:15; Amu 7:24-25; Kut 15:14
[e]**3:8** Kut 7:20; 14:21, 22; 2Fal 2:11; Za 77:16; 68:17
[f]**3:9** Kum 32:23; Za 7:12-13
[g]**3:10** Za 77:16; 98:7; 93:3
[h]**3:11** Yos 10:13; Za 18:14; 144:6; Zek 9:14
[i]**3:12** Za 44:2, 3; Mik 4:13; Isa 41:15
[j]**3:13** Kut 13:21; Za 20:6; 28:8; 68:21; 2Sam 5:20; 23:1
[k]**3:14** Amu 7:22; Za 64:2-5
[l]**3:15** Ay 9:8; Kut 15:8
[m]**3:16** Ay 4:14; Za 37:7
[n]**3:17** Yoe 1:10-18; 2Kor 4:8, 9; Yer 5:17

18 [a]hata hivyo nitashangilia katika
BWANA,
nitamfurahia Mungu Mwokozi
wangu.

19 [b]BWANA Mwenyezi ni nguvu yangu;
huifanya miguu yangu kama
miguu ya ayala,
huniwezesha kupita juu ya vilima.

Kwa kiongozi wa uimbaji. Kwa
vinanda vyangu vya nyuzi.

---

[a]**3:18** Za 42:5; 97:12; Isa 61:10; Kut 15:2; Lk 1:47; Flp 4:4

[b]**3:19** Kum 32:13; 33:29; Za 27:1; 46:1-5; 18:33

# SEFANIA

1 [a]Neno la BWANA lililomjia Sefania mwana wa Kushi, mwana wa Gedalia, mwana wa Amaria, mwana wa Hezekia, wakati wa utawala wa Yosia mwana wa Amoni mfalme wa Yuda:

*Onyo La Maangamizi Yanayokuja*

2 [b]BWANA asema,
“Nitafagia kila kitu
kutoka kwenye uso wa dunia.”
3 [c]“Nitafagilia mbali watu na wanyama;
nitafagilia mbali ndege wa angani
na samaki wa baharini.
Wafanyao maovu watapata tu kokoto,
nami nitamkatilia mbali mwanadamu atoke katika dunia,”
asema BWANA.

*Dhidi Ya Yuda*

4 [d]“Nitaiadhibu Yuda
na wote wakaao Yerusalemu.
Kutoka mahali hapa nitakatilia mbali
kila mabaki ya Baali,
majina ya wapagani na makuhani
waabuduo sanamu:
5 [e]wale ambao husujudu juu ya mapaa
kuabudu jeshi la vitu vya angani,
wale ambao husujudu na kuapa kwa BWANA
na ambao pia huapa kwa Malkamu,
6 [f]wale wanaoacha kumfuata BWANA,
wala hawamtafuti BWANA
wala kutaka shauri lake.
7 [g]Nyamazeni mbele za BWANA Mwenyezi,
kwa maana siku ya BWANA iko karibu.
BWANA ameandaa dhabihu,
amewaweka wakfu wale aliowaalika.
8 [h]Katika siku ya dhabihu ya BWANA
nitawaadhibu wakuu
na wana wa mfalme
na wale wote wanaovaa
nguo za kigeni.
9 [i]Katika siku hiyo nitaadhibu wote ambao
hukwepa kukanyaga kizingiti,
ambao hujaza hekalu la miungu yao
kwa dhuluma na udanganyifu.”

10 [j]BWANA asema, “Katika siku hiyo
kilio kitapanda juu kutoka lango la Samaki,
maombolezo kutoka mtaa wa pili,
na mshindo mkubwa kutoka vilimani.
11 [k]Ombolezeni, ninyi mnaoishi katika eneo la sokoni;
wafanyabiashara wenu wote wameangamizwa,
wote ambao wanafanya biashara ya fedha
wataangamizwa.
12 [l]Wakati huo nitasaka mji wa Yerusalemu kwa taa,
na kuwaadhibu wale ambao
wanakaa katika hali ya kuridhika,
ambao ni kama divai
iliyobaki kwenye machicha,

---

[a]**1:1** 2Fal 22:1; 2Tim 3:16; 2Pet 1:21; 1Nya 3:14
[b]**1:2** Mwa 6:7
[c]**1:3** Yer 4:25; 50:3; Hos 4:3; Eze 14:17
[d]**1:4** Yer 6:12; 15:6; Mik 5:13; Sef 2:11; Hos 10:5
[e]**1:5** Yer 5:7; 8:2; 1Fal 11:33; Law 18:21
[f]**1:6** Yer 2:13; Isa 9:13; Hos 7:7
[g]**1:7** Isa 13:6; 41:1; Eze 7:19; Yoe 3:14; Amo 5:18-20; Yer 46:10
[h]**1:8** Isa 24:21; Yer 39:6
[i]**1:9** 1Sam 5:5; Amo 3:10
[j]**1:10** Isa 22:5; Neh 3:13; 2Nya 33:14; Amo 5:16
[k]**1:11** Yak 5:1; Hos 9:6; Ufu 18:11, 12
[l]**1:12** Amo 6:1; Ay 21:15; Za 10:11-13; Yer 48:11; Eze 8:12; 2Fal 21:16; Ay 22:13

ambao hudhani, 'BWANA hatafanya lolote,
jema au baya.'
13 [a]Utajiri wao utatekwa nyara,
nyumba zao zitabomolewa.
Watajenga nyumba,
lakini hawataishi ndani yake;
watapanda mizabibu
lakini hawatakunywa divai yake.

*Siku Kubwa Ya Bwana*

14 [b]"Siku kubwa ya BWANA iko karibu:
iko karibu na inakuja haraka.
Sikilizeni! Kilio katika siku ya BWANA
kitakuwa kichungu,
hata shujaa atapiga kelele.
15 [c]Siku ile ni siku ya ghadhabu,
siku ya fadhaa na dhiki,
siku ya uharibifu na ukiwa,
siku ya giza na utusitusi,
siku ya mawingu na giza nene,
16 [d]siku ya tarumbeta na mlio wa vita
dhidi ya miji yenye ngome
na dhidi ya minara mirefu.
17 [e]Nitawaletea watu dhiki,
nao watatembea kama vipofu,
kwa sababu wametenda dhambi
dhidi ya BWANA.
Damu yao itamwagwa kama vumbi
na matumbo yao kama taka.
18 [f]Fedha yao wala dhahabu yao
hazitaweza kuwaokoa
katika siku hiyo ya ghadhabu ya BWANA.
Katika moto wa wivu wake
dunia yote itateketezwa,
kwa maana ataleta mwisho
wa wote wanaoishi katika dunia ghafula."

2 1 [g]Kusanyikeni pamoja, kusanyikeni pamoja,
enyi taifa lisilo na aibu,
2 [h]kabla ya wakati ulioamriwa haujafika
na siku ile inayopeperusha kama makapi,
kabla hasira kali ya BWANA haijaja juu yenu,
kabla siku ya ghadhabu ya BWANA
haijaja juu yenu.
3 [i]Mtafuteni BWANA, enyi nyote wanyenyekevu wa nchi,
ninyi ambao hufanya lile analoamuru.
Tafuteni haki, tafuteni unyenyekevu;
labda mtahifadhiwa
siku ya hasira ya BWANA.

*Dhidi Ya Ufilisti*

4 [j]Gaza utaachwa
na Ashkeloni utaachwa magofu.
Wakati wa adhuhuri Ashdodi utaachwa mtupu
na Ekroni utang'olewa.
5 [k]Ole wenu ninyi ambao mnaishi kando ya bahari,
enyi Wakerethi;
neno la BWANA liko dhidi yenu,
ee Kanaani, nchi ya Wafilisti.

"Mimi nitawaangamiza,
na hakuna atakayebaki."

6 [l]Nchi kando ya bahari, mahali ambapo wanaishi Wakerethi,
patakuwa mahali pa wachungaji
na mazizi ya kondoo.

---

[a]**1:13** 2Fal 24:13; Yer 15:13; Mik 6:15; Kum 28:30-39; Mao 5:2; Amo 5:11
[b]**1:14** Yer 30:7; Ufu 6:17; Yoe 1:15; 2:1; Mal 4:5; Eze 7:7; Dan 7:13
[c]**1:15** 1Sam 2:9; Mk 13:24-25; Yoe 2:2
[d]**1:16** Yer 4:19; 8:16; Hos 5:8; Amo 3:6; Kum 28:52; Isa 2:15
[e]**1:17** Kum 28:52; Isa 59:10; Yer 9:22; Za 79:3; 83:10
[f]**1:18** Ay 20:20; 40:11; Eze 7:11; 7:19; Kum 29:20; Sef 3:8; Mwa 6:7
[g]**2:1** 2Nya 20:4; Yoe 1:14; 2:16; Yer 3:3; 6:15
[h]**2:2** Isa 17:13; Hos 13:3; 2Fal 23:26; Yer 4:4; 10:25; Eze 7:19; Mao 4:11
[i]**2:3** Amo 5:6; Yoe 2:4; Isa 1:17; Za 45:4; 57:1; 76:9
[j]**2:4** Mwa 10:19; Amo 1:6-8; Zek 9:5-7; Yer 6:4; 47:5
[k]**2:5** 1Sam 30:14; Law 26:31; Eze 25:16; Yos 13:3; Isa 14:30
[l]**2:6** Isa 5:17; 17:2

7 [a]Itakuwa mali ya mabaki ya nyumba
ya Yuda,
hapo watapata malisho.
Wakati wa jioni watajilaza chini
katika nyumba za Ashkeloni.
BWANA Mungu wao atawatunza,
naye atawarudishia wafungwa
wao.

*Dhidi Ya Moabu Na Amoni*

8 [b]"Nimeyasikia matukano ya Moabu
nazo dhihaka za Waamoni,
ambao waliwatukana watu wangu
na kutoa vitisho dhidi ya nchi yao.
9 [c]Hakika, kama niishivyo,"
asema BWANA Mwenye Nguvu
Zote,
Mungu wa Israeli,
"hakika Moabu itakuwa kama
Sodoma,
Waamoni kama Gomora:
mahali pa magugu na mashimo ya
chumvi,
nchi ya ukiwa milele.
Mabaki ya watu wangu watawateka
nyara;
mabaki ya taifa langu watarithi
nchi yao."

10 [d]Hiki ndicho watarudishiwa kwa ajili
ya kiburi chao,
kwa kutukana na kudhihaki
watu wa BWANA Mwenye Nguvu
Zote.
11 [e]BWANA atakuwa wa kuhofisha kwao
atakapoangamiza miungu yote ya
nchi.
Mataifa katika kila pwani
yatamwabudu,
kila moja katika nchi yake.

*Dhidi Ya Kushi*

12 [f]"Ninyi pia, ee Wakushi,
mtauawa kwa upanga wangu."

*Dhidi Ya Ashuru*

13 [g]Mungu atanyoosha mkono wake
dhidi ya kaskazini
na kuangamiza Waashuru,
akiiacha Ninawi ukiwa
na pakame kama jangwa.
14 [h]Makundi ya kondoo na ng'ombe
yatajilaza pale,
viumbe vya kila aina.
Bundi wa jangwani na bundi waliao
kwa sauti nyembamba
wataishi juu ya nguzo zake.
Mwangwi wa kuita kwao utapita
madirishani,
kifusi kitakuwa milangoni,
boriti za mierezi zitaachwa wazi.
15 [i]Huu ndio mji uliotukuka na kuishi
kwa furaha
wakijisikia salama.
Ulisema moyoni mwako,
"Mimi ndimi, na wala hapana
mwingine ila mimi."
Jinsi gani umekuwa gofu,
mahali pa kulala wanyama pori!
Wote wanaopita kando yake
wanauzomea
na kutikisa mkono kwa dharau.

*Hatima Ya Yerusalemu*

3 [j]Ole mji wa wadhalimu,
waasi na waliotiwa unajisi!
2 [k]Hautii mtu yeyote,
haukubali maonyo.

[a]**2:7** Isa 11:11; Hag 1:12; Mik 5:7; 4:10; Kut 4:31; Lk 1:68; Mwa 45:7; Kum 30:3; Za 126:4; Yer 23:3; 32:44; Hos 6:11; Eze 39:25; Yoe 3:1; Amo 1:6-8
[b]**2:8** Mwa 19:37; Yer 48:27; 49:1; Eze 25:3, 8; 21:28; Mao 3:61; Isa 16:6
[c]**2:9** Kum 23:6; 29:23; Isa 11:14; Yer 48:1-47; 49:1-6; Eze 25:1-11; 2Fal 19:31; Amo 1:13; 2:1-3
[d]**2:10** Ay 40:12; Isa 16:6; Yer 48:27; Za 9:6
[e]**2:11** Mwa 49:10; 10:5; Za 2:8; 22:27; Isa 2:2, 3; Mal 1:11; Yn 4:21; 1Tim 2:8; Yoe 2:11; 1Nya 19:1; Eze 25:6-7; Isa 12:4; Za 86:9; Sef 3:9
[f]**2:12** Mwa 10:6; Isa 18:1; 20:4; Yer 46:10
[g]**2:13** Mwa 10:5-11; Zek 10:11; Mik 5:6
[h]**2:14** Isa 5:17; 13:21; 14:23; Ufu 18:2; Za 102:6
[i]**2:15** Isa 32:9; 47:8; Eze 27:36; 28:2; Ufu 18:7; Yer 49:33; Nah 3:19
[j]**3:1** Yer 6:6; Kum 21:18; Eze 23:30
[k]**3:2** Yer 5:3; 7:28; 22:21; Kum 1:32; Law 26:33; Za 78:23

Haumtumaini BWANA,
haukaribii karibu na Mungu wake.
3 [a]Maafisa wake ni simba
wangurumao,
watawala wake ni mbwa mwitu
wa jioni,
ambao hawabakizi chochote
kwa ajili ya asubuhi.
4 [b]Manabii wake ni wenye kiburi,
ni wadanganyifu.
Makuhani wake hunajisi patakatifu
na kuihalifu sheria.
5 [c]BWANA aliye ndani yake ni mwenye
haki,
hafanyi kosa.
Asubuhi kwa asubuhi hutoa haki
yake,
kila kukipambazuka huitimiza,
bali mtu dhalimu hana aibu.

6 [d]"Nimeyafutilia mbali mataifa,
ngome zao zimebomolewa.
Nimeziacha barabara ukiwa,
hakuna anayepita humo.
Miji yao imeharibiwa;
hakuna mmoja atakayeachwa:
hakuna hata mmoja.
7 [e]Niliuambia huo mji,
'Hakika utaniogopa na kukubali
maonyo!'
Ndipo makao yake hayatafutiliwa
mbali,
wala adhabu zangu zote
hazitakuja juu yake.
Lakini walikuwa bado na shauku
kutenda kwa upotovu katika yote
waliyofanya."
8 [f]BWANA anasema,
"Kwa hiyo ningojee mimi,
siku nitakayosimama kuteka
nyara.
Nimeamua kukusanya mataifa,
kukusanya falme
na kumimina ghadhabu yangu juu
yao,
hasira yangu kali yote.
Dunia yote itateketezwa
kwa moto wa wivu wa hasira
yangu.

9 [g]"Ndipo nitatakasa midomo ya
mataifa,
kwamba wote waweze kuliitia jina
la BWANA
na kumtumikia kwa pamoja.
10 [h]Kutoka ng'ambo ya mito ya Kushi
watu wangu wanaoniabudu,
watu wangu waliotawanyika,
wataniletea sadaka.
11 [i]Siku hiyo hutaaibishwa
kwa ajili ya makosa yote
ulionitendea,
kwa sababu nitawaondoa kutoka mji
huu
wale wote wanaoshangilia
katika kiburi chao.
Kamwe hutajivuna tena
katika kilima changu kitakatifu.
12 [j]Lakini nitakuachia ndani yako
wapole na wanyenyekevu,
ambao wanatumaini jina la
BWANA.
13 [k]Mabaki ya Israeli hayatafanya kosa;
hawatasema uongo,
wala udanganyifu hautakuwa
katika vinywa vyao.
Watakula na kulala
wala hakuna yeyote
atakayewaogopesha."

14 [l]Imba, ee Binti Sayuni;
paza sauti, ee Israeli!

---

[a]**3:3** Za 22:13; Mwa 49:27; Mik 3:3
[b]**3:4** Za 25:3; Isa 48:8; Yer 3:20; 9:4; 23:11; Mal 2:10; Eze 22:26
[c]**3:5** Ezr 9:15; Kum 32:4; Za 5:3; 99:3, 4; Mao 3:23; Yer 3:3; Eze 18:25
[d]**3:6** Law 26:31
[e]**3:7** Yer 7:28; Mwa 6:12; Hos 9:9
[f]**3:8** Za 27:14; 79:6; Yoe 3:2; 3:11; Isa 2:3; Mit 20:22; Ufu 16:1; Yer 10:25; Mao 4:11; Sef 1:18
[g]**3:9** Sef 2:11; Mwa 4:26; Isa 19:18
[h]**3:10** Mwa 10:6; Za 68:31; Mal 1:11; Isa 60:7; Mdo 8:27; 2Nya 32:23
[i]**3:11** Isa 29:22; Yoe 2:26-27; Mwa 50:15; Kut 15:17; Za 59:12; Mt 3:9; Law 26:19
[j]**3:12** Isa 14:32; Mt 5:3; Lk 6:20; Isa 57:15; Yer 29:12; Nah 1:7
[k]**3:13** Isa 4:3; 10:21; Za 119:3; Yer 33:16; Ufu 14:5; Ay 16:17; Eze 34:25-28
[l]**3:14** Za 9:14; 14:7; Zek 2:10; Isa 12:6; 51:11

Furahi na kushangilia kwa moyo
wako wote,
ee Binti Yerusalemu!
15 [a]BWANA amekuondolea adhabu
yako,
amewarudisha nyuma adui zako.
BWANA, Mfalme wa Israeli, yu
pamoja nawe;
kamwe hutaogopa tena madhara
yoyote.
16 [b]Katika siku hiyo watauambia
Yerusalemu,
"Usiogope, ee Sayuni;
usiiache mikono yako ilegee.
17 [c]BWANA Mungu wako yu pamoja
nawe,
yeye ni mwenye nguvu kuokoa.
Atakufurahia kwa furaha kubwa,
atakutuliza kwa pendo lake,
atakufurahia kwa kuimba."

18 [d]"Huzuni katika sikukuu
zilizoamriwa
nitaziondoa kwenu;
hizo ni mzigo na fedheha kwenu.
19 [e]Wakati huo nitawashughulikia
wote waliokudhulumu;
nitaokoa vilema na kukusanya
wale ambao wametawanywa.
Nitawapa sifa na heshima
katika kila nchi ambayo
waliaibishwa.
20 [f]Wakati huo nitawakusanya;
wakati huo nitawaleta nyumbani.
Nitawapa sifa na heshima
miongoni mwa mataifa yote ya
dunia
wakati nitakapowarudishia mateka
yenu
mbele ya macho yenu hasa,"
asema BWANA.

---

[a]**3:15** Yn 1:49; Eze 37:26-28; 48:35; Ufu 21:3; Isa 54:14; Zek 9:9
[b]**3:16** 2Fal 19:26; Ebr 12:12; Ay 4:3; Isa 35:3-4
[c]**3:17** Isa 40:1; 62:4; 63:1; Yoe 2:21; Kum 28:63; Hos 14:4
[d]**3:18** Mao 2:6
[e]**3:19** Isa 14:2; 60:18; Eze 34:16; Mik 4:6
[f]**3:20** Yer 29:14; Eze 37:12; Za 22:27; Isa 56:5; 60:18; 66:22; Kum 26:19

# HAGAI

*Wito Wa Kuijenga Nyumba Ya Bwana*

1 [a]Katika mwaka wa pili wa utawala wa
Mfalme Dario wa Uajemi, katika siku ya
kwanza ya mwezi wa sita, neno la BWANA
lilikuja kupitia kwa nabii Hagai kwenda
kwa Zerubabeli mwana wa Shealtieli,
mtawala wa Yuda na kwa Yoshua[b] mwana
wa kuhani mkuu Yehosadaki:
2 [c]Hivi ndivyo asemavyo BWANA Mwenye
Nguvu Zote: "Hawa watu husema, 'Wakati
haujawadia wa kujenga nyumba ya
BWANA.' "
3 [d]Kisha neno la BWANA likaja kupitia kwa
nabii Hagai: 4 [e]"Je, ni wakati wenu ninyi wa
kuishi katika nyumba zenu zilizojengwa
vizuri, wakati hii nyumba ikibaki, gofu?"
5 [f]Sasa hili ndilo asemalo BWANA Mwenye
Nguvu Zote: "Zitafakarini vyema njia zenu.
6 [g]Mmepanda vingi, lakini mmevuna haba.
Mnakula lakini hamshibi, mnakunywa,
lakini hamtosheki. Mnavaa nguo, lakini
hamsikii joto. Mnapata mishahara, lakini
inatoweka kama imewekwa kwenye mfuko
uliotobokatoboka."
7 Hili ndilo asemalo BWANA Mwenye
Nguvu Zote: "Zitafakarini vyema njia
zenu. 8 [h]Pandeni milimani mkalete miti na
kujenga nyumba, ili nipate kuifurahia, na
nitukuzwe," asema BWANA. 9 [i]"Mlitarajia
mengi, kumbe, yametokea kidogo.
Ulichokileta nyumbani nilikipeperusha.
Kwa nini?" asema BWANA Mwenye Nguvu
Zote. "Ni kwa sababu ya nyumba yangu,
inayobaki katika hali ya magofu, wakati
kila mmoja wenu anajishughulisha na
nyumba yake mwenyewe. 10 [j]Kwa hiyo,
kwa sababu yenu mbingu zimezuia umande
wake na ardhi mavuno yake. 11 [k]Niliita
ukame mashambani na milimani, kwenye
nafaka, mvinyo mpya, mafuta pamoja na
chochote kinachozalishwa na ardhi, juu
ya watu na ng'ombe, pamoja na kazi za
mikono yenu."

12 [l]Kisha Zerubabeli mwana wa
Shealtieli, Yoshua kuhani mkuu mwana
wa Yehosadaki, pamoja na mabaki yote
ya watu wakaitii sauti ya BWANA Mungu
wao pamoja na ujumbe wa nabii Hagai,
kwa sababu alikuwa ametumwa na BWANA
Mungu wao. Watu walimwogopa BWANA.
13 [m]Kisha Hagai, mjumbe wa BWANA,
akawapa watu ujumbe huu wa BWANA:
"Mimi niko pamoja nanyi," asema BWANA.
14 [n]Kwa hiyo BWANA akachochea roho ya
Zerubabeli mwana wa Shealtieli, mtawala
wa Yuda, na roho ya kuhani mkuu Yoshua
mwana wa Yehosadaki, pamoja na roho za
mabaki yote ya watu. Walikuja wakaanza
kufanya kazi katika nyumba ya BWANA
Mwenye Nguvu Zote, Mungu wao, 15 [o]katika
siku ya ishirini na nne mwezi wa sita, katika
mwaka wa pili wa utawala wa Mfalme
Dario.

*Utukufu Ulioahidiwa Wa Nyumba Mpya*

2 [p]Katika siku ya ishirini na moja ya
mwezi wa saba, neno la BWANA lilikuja

[a]**1:1** Ezr 4:24; 5:1-3; 2:2; 3:2; 1Nya 3:19; 6:15; Mt 1:12-13
[b]1 Yoshua kwa Kiebrania ni Yeshua, maana yake ni Yehova ni wokovu.
[c]**1:2** Isa 13:4; 29:13
[d]**1:3** Ezr 5:1
[e]**1:4** 2Sam 7:2; Yer 33:12
[f]**1:5** Mao 3:40; Hag 2:15-18
[g]**1:6** Law 26:20; Isa 5:10; 9:20; 55:2; Amo 4:8; Hag 2:16; Zek 8:10
[h]**1:8** Ay 22:3; Yer 13:11; 1Nya 14:1; Za 132:13-14; Kut 29:43
[i]**1:9** Kum 28:38; Isa 5:10; Neh 13:11; Za 103:16; Eze 22:21
[j]**1:10** Kum 28:24; Mwa 27:28; 1Fal 17:1; 2Nya 6:26; Yer 3:3; Law 26:19; Yoe 1:18-19
[k]**1:11** Kum 11:26; 28:22; Rut 1:1; 1Fal 17:1; Hag 2:17; Isa 5:6; 7:25; Hes 18:12
[l]**1:12** Isa 1:9; 50:10; 55:11; Mt 28:20; Kum 31:12; Hag 2:2; Ezr 5:2; Mhu 12:13; Ay 36:11
[m]**1:13** Hes 14:9; 27:21; 2Nya 15:2; 36:15; Mwa 26:3; Rum 8:31; Isa 41:10; Mt 28:20
[n]**1:14** Ezr 5:2; Za 110:3; 2Nya 36:22; Hag 2:21; 1Nya 6:15; 1Kor 15:58
[o]**1:15** Hag 2:10, 20; Ezr 4:24
[p]**2:1** Law 23:34; Yn 7:37; Ezr 5:1

kupitia nabii Hagai, kusema: 2 [a]“Sema na
Zerubabeli mwana wa Shealtieli, mtawala
wa Yuda, kuhani mkuu Yoshua mwana wa
Yehosadaki, na mabaki ya watu. Uwaulize,
3 [b]‘Ni nani miongoni mwenu aliyebaki
ambaye aliiona hii nyumba katika utukufu
wake wa mwanzo? Sasa inaonekanaje
kwenu? Je, haionekani kwenu kama si kitu?
4 [c]Lakini sasa uwe imara, ee Zerubabeli,’
asema Bwana. ‘Kuwa imara, ee kuhani
mkuu Yoshua mwana wa Yehosadaki. Mwe
imara, enyi watu wote wa nchi,’ asema
Bwana, ‘na mfanye kazi. Kwa kuwa mimi
nipo pamoja nanyi,’ asema Bwana Mwenye
Nguvu Zote. 5 [d]“Hili ndilo nililoagana nanyi
mlipotoka katika nchi ya Misri. Pia Roho
wangu anadumu katikati yenu. Msiogope.’

6 [e]“Hili ndilo asemalo Bwana Mwenye
Nguvu Zote: ‘Baada ya muda kidogo kwa
mara nyingine nitazitikisa mbingu na
nchi, bahari na nchi kavu. 7 [f]Nitatikisa
mataifa yote, nacho kile kinachotamaniwa
na mataifa yote kitakuja, nami nitaujaza
utukufu katika nyumba hii,’ asema Bwana
Mwenye Nguvu Zote. 8 [g]‘Fedha ni mali
yangu na dhahabu ni mali yangu,’ asema
Bwana Mwenye Nguvu Zote. 9 [h]‘Utukufu wa
nyumba hii ya sasa utakuwa mkubwa kuliko
utukufu wa ile nyumba ya mwanzoni,’
asema Bwana Mwenye Nguvu Zote. ‘Na
mahali hapa nitawapa amani,’ asema
Bwana Mwenye Nguvu Zote.”

### *Baraka Kwa Watu Waliotiwa Unajisi*

10 [i]Katika siku ya ishirini na nne ya mwezi
wa tisa, katika mwaka wa pili wa utawala
wa Mfalme Dario, neno la Bwana lilikuja
kwa nabii Hagai: 11 [j]“Hili ndilo asemalo
Bwana Mwenye Nguvu Zote: ‘Ulizeni
makuhani jinsi sheria inavyosema: 12 [k]Kama
mtu akibeba nyama iliyowekwa wakfu
katika pindo la vazi lake, kisha lile pindo
likagusa mkate au mchuzi, divai, mafuta
au chakula kingine, je, kitu hicho kitakuwa
kimewekwa wakfu?’ ”

Makuhani wakajibu, “La hasha.”

13 [l]Kisha Hagai akasema, “Je, kama mtu
aliyetiwa unajisi kwa kugusa maiti akigusa
mojawapo ya vitu hivi, kitu hicho kitakuwa
kimetiwa unajisi?”

Makuhani wakajibu, “Ndiyo, huwa
kimenajisiwa.”

14 [m]Kisha Hagai akasema, “ ‘Basi ndivyo
walivyo machoni pangu hawa watu na taifa
hili,’ asema Bwana. ‘Lolote wafanyalo na
chochote watoacho hapo ni najisi.

15 [n]“ ‘Sasa fikirini kwa uangalifu kuanzia
leo na kuendelea: tafakarini jinsi mambo
yalivyokuwa kabla halijawekwa jiwe moja
juu ya lingine katika Hekalu la Bwana.
16 [o]Wakati mtu alipoendea lundo la nafaka
la vipimo ishirini, kulikuwa na vipimo kumi
tu. Wakati mtu alipoendea pipa la mvinyo
ili kuchota vipimo hamsini, kulikuwa na
vipimo ishirini tu. 17 [p]Kazi zenu zote za
mikono nilizipiga kwa ukame, ukungu
na mvua ya mawe, lakini hata hivyo,
hamkunigeukia mimi,’ asema Bwana.
18 [q]‘Tangu leo na kuendelea, kuanzia siku
hii ya ishirini na nne ya mwezi wa tisa,
tafakarini siku ambayo msingi wa Hekalu
la Bwana uliwekwa. Tafakarini: 19 [r]Je,
bado kuna mbegu iliyobakia ghalani?

---

[a]**2:2** Hag 1:12; 1Nya 6:15
[b]**2:3** Ezr 3:12; Isa 60:7; Zek 4:10
[c]**2:4** Zek 8:9; Hag 1:13; 1Sam 16:18; Mk 16:20; Rum 8:31; 1Nya 28:20; Efe 6:10; Kut 3:12; 33:14; Hes 14:9; Mdo 7:9; 2Sam 5:10
[d]**2:5** Mwa 6:18; 15:1; Kut 29:46; Neh 9:20; Zek 4:6; 8:13; Isa 63:11; Ezr 5:2; 1Nya 28:20
[e]**2:6** Kut 19:18; Ay 9:6; Isa 10:25; 14:16; 34:4; Eze 38:19; Yer 4:26; Ebr 12:26
[f]**2:7** 1Sam 9:20; Isa 60:7; Mwa 3:15; Kum 18:15; Za 24:7; Lk 2:32; Kut 16:7; 29:43
[g]**2:8** 1Nya 29:2
[h]**2:9** Za 85:9; Isa 9:6; 11:10; 60:7, 17; Law 26:6; Ezr 3:12; Lk 11:31; 2:14; Yn 1:14
[i]**2:10** Hag 1:15
[j]**2:11** Law 10:10-11; Kum 17:8-11; 33:8; Yer 18:18
[k]**2:12** Yer 11:15; Mwa 7:2
[l]**2:13** Law 22:4-6; Hes 19:13
[m]**2:14** Isa 1:13; 29:13; Tit 1:14-15; Za 51:17
[n]**2:15** Ezr 3:10; 4:24; Hag 1:5
[o]**2:16** Rut 3:7; Ay 24:11; Isa 5:2, 10; Hag 1:6; Kum 28:38
[p]**2:17** Hag 1:11; Kut 9:18; Kum 28:22; Za 78:48; Isa 9:13; Amo 4:6; 1Fal 8:37; Yer 3:10; 5:3
[q]**2:18** Zek 8:9; Hag 1:5; Ezr 3:11
[r]**2:19** Kut 28:33; Yoe 1:12; 2:14; Mwa 12:2; Law 25:21; Za 128:1-6

Mpaka sasa, hakuna mzabibu au mtini, mkomamanga wala mzeituni uliozaa tunda.
" 'Kuanzia leo na kuendelea, nitawabariki.' "

*Zerubabeli Pete Ya Muhuri Ya Bwana*

20 [a]Neno la BWANA likamjia Hagai kwa
mara ya pili katika siku ya ishirini na nne
ya mwezi kusema: 21 [b]"Mwambie Zerubabeli
mtawala wa Yuda kwamba nitazitikisa
mbingu na nchi. 22 [c]Nitapindua viti vya
enzi vya falme, na kuziharibu kabisa nguvu za falme za kigeni. Nitapindua magari ya vita pamoja na waendeshaji wake; farasi na wapanda farasi wataanguka, kila mmoja kwa upanga wa ndugu yake.
23 [d]" 'Katika siku ile,' asema BWANA Mwenye Nguvu Zote, 'nitakuchukua wewe, mtumishi wangu Zerubabeli mwana wa Shealtieli,' asema BWANA. 'Nitakufanya kama pete yangu ya muhuri, kwa kuwa nimekuchagua,' asema BWANA Mwenye Nguvu Zote."

---

[a]**2:20** Ezr 1:5; Hag 1:15
[b]**2:21** Ezr 5:2; Isa 14:16; Eze 21:27; 38:19-20; Ebr 12:26
[c]**2:22** Mwa 19:25; Ay 2:13; Dan 2:44; Mik 5:10; Mt 24:7; Kut 15:21; Eze 38:21; Amu 7:22
[d]**2:23** Zek 4:10; Kut 28:9; Dan 9:24-26; Mwa 38:18; 2Kor 1:22; Mt 1:12; Wim 8:6; Yer 22:24; Isa 2:11; 10:20; 20:3; 2:1

# ZEKARIA

*Wito Wa Kumrudia Bwana*

1 [a]Katika mwezi wa nane wa mwaka wa
pili wa utawala wa Mfalme Dario, neno
la BWANA lilimjia nabii Zekaria mwana wa
Berekia, mwana wa Ido, kusema:
2 [b]“BWANA aliwakasirikia sana baba zako
wa zamani. 3 [c]Kwa hiyo waambie watu:
Hivi ndivyo BWANA Mwenye Nguvu Zote
asemavyo: ‘Nirudieni mimi,’ asema BWANA
Mwenye Nguvu Zote, ‘nami nitawarudia
ninyi,’ asema BWANA Mwenye Nguvu
Zote. 4 [d]Msiwe kama baba zenu, ambao
manabii waliotangulia waliwatangazia:
Hivi ndivyo BWANA Mwenye Nguvu Zote
asemavyo: ‘Geukeni, mziache njia zenu
mbaya na matendo yenu maovu.’ Lakini
hawakunisikiliza wala kufuata maelekezo
yangu, asema BWANA. 5 Wako wapi baba
zako sasa? Nao manabii, je, wanaishi
milele? 6 [e]Je, maneno yangu na amri zangu
nilizowaagiza manabii watumishi wangu,
hayakuwapata baba zenu?”

“Kisha walitubu na kusema, ‘BWANA
Mwenye Nguvu Zote ametutenda sawasawa
na njia zetu na matendo yetu yalivyostahili,
kama alivyokusudia kufanya.’ ”

*Maono Ya Kwanza: Mtu Katikati Ya Miti Ya Mihadasi*

7 Katika siku ya ishirini na nne ya mwezi
wa kumi na moja, yaani mwezi uitwao
Shebati, katika mwaka wa pili wa utawala
wa Mfalme Dario, neno la BWANA lilimjia
nabii Zekaria mwana wa Berekia mwana
wa Ido.

8 [f]Wakati wa usiku nilipata maono,
mbele yangu alikuwepo mtu akiendesha
farasi mwekundu! Alikuwa amesimama
katikati ya miti ya mihadasi kwenye bonde.
Nyuma yake walikuwepo farasi wekundu,
wa kikahawia na weupe.
9 [g]Nikauliza, “Hivi ni vitu gani bwana
wangu?”

Malaika aliyekuwa akizungumza na mimi
akanijibu, “Nitakuonyesha kuwa ni nini.”
10 [h]Kisha yule mtu aliyesimama katikati ya
miti ya mihadasi akaeleza, “Ni wale ambao
BWANA amewatuma waende duniani kote.”
11 [i]Nao wakatoa taarifa kwa yule malaika
wa BWANA, aliyekuwa amesimama katikati
ya miti ya mihadasi, “Tumepita duniani kote
na kukuta ulimwengu wote umepumzika
kwa amani.”
12 [j]Kisha malaika wa BWANA akasema,
“BWANA Mwenye Nguvu Zote, utazuia
mpaka lini rehema kutoka Yerusalemu na
miji ya Yuda, ambayo umeikasirikia kwa
miaka hii sabini?” 13 [k]Kwa hiyo BWANA
akazungumza maneno ya upole na ya
kufariji kwa malaika aliyezungumza nami.
14 [l]Kisha malaika yule aliyekuwa
akizungumza nami akasema, “Tangaza
neno hili: Hili ndilo BWANA Mwenye
Nguvu Zote asemalo: ‘Nina wivu sana
kwa ajili ya Yerusalemu na Sayuni,
15 [m]lakini nimeyakasirikia sana mataifa
yanayojisikia kuwa yako salama. Nilikuwa
nimewakasirikia Israeli kidogo tu, lakini
mataifa hayo yaliwazidishia maafa.’
16 [n]“Kwa hiyo, hivi ndivyo asemavyo

[a]**1:1** Ezr 4:24; 6:15; Mt 23:35; Lk 11:51; Neh 12:4
[b]**1:2** 2Nya 36:16
[c]**1:3** Yak 4:8; Mal 3:7; Ay 22:2; Yer 25:5; Mik 7:19; Lk 15:20
[d]**1:4** 2Nya 7:14; 24:19; 36:15; Zek 7:7; 2Fal 17:13; Za 78:8; 106:6; Yer 6:17; 17:23; 23:22; Eze 20:18; 33:4; Isa 1:16-17; Yer 3:12; Eze 33:11; Hos 14:1; Mit 3:8-9; Mdo 3:19
[e]**1:6** Isa 44:26; Kum 28:2; Dan 9:12; Hos 5:9; Yer 12:14-17; 39:16; 23:20; 44:17; Mao 2:17; Isa 55:1; Mao 1:18
[f]**1:8** Ufu 6:4; Zek 6:2-7; Yos 5:13
[g]**1:9** Zek 4:1-5; 5:5; Dan 7:16
[h]**1:10** Zek 6:5-8; Za 91:11; Ebr 1:14
[i]**1:11** Isa 14:7; Mwa 16:7; Za 102:20
[j]**1:12** Za 6:3; 40:11; Yer 40:5; 2Nya 36:21; Dan 9:2; Za 103:13; Ufu 6:10; Zek 7:5
[k]**1:13** Isa 35:4; Ay 15:11; Zek 4:1; Isa 40:1-2; Yer 29:10
[l]**1:14** Isa 26:11; Yoe 2:18; Zek 8:2
[m]**1:15** Yer 48:11; 2Nya 28:9; Za 69:26; 123:3-4; Amo 1:11; Isa 47:6
[n]**1:16** Zek 2:1-2; 8:3; Ay 38:5; Isa 12:1

Bwana: ‘Nitairudia Yerusalemu kwa
rehema na huko nyumba yangu itajengwa
tena. Nayo kamba ya kupimia itanyooshwa
Yerusalemu,’ asema Bwana Mwenye
Nguvu Zote.
[17] [a]“Endelea kutangaza zaidi kwamba:
Hivi ndivyo asemavyo Bwana Mwenye
Nguvu Zote: ‘Miji yangu itafurika tena
ustawi na Bwana atamfariji tena Sayuni
na kumchagua Yerusalemu.’ ”

*Maono Ya Pili: Pembe Nne Na Mafundi Wanne*

[18] Kisha nikatazama juu, na pale mbele
yangu nikaona pembe nne! [19] [b]Nikamuuliza
yule malaika aliyekuwa akizungumza nami,
“Ni nini hivi?”
Akanijibu, “Hizi ni zile pembe
zilizowatawanya Yuda, Israeli na
Yerusalemu.”
[20] Kisha Bwana akanionyesha mafundi
wanne. [21] [c]Nikauliza, “Hawa wanakuja
kufanya nini?”
Akanijibu, “Hizi ndizo pembe
zilizowatawanya Yuda ili asiwepo
atakayeweza kuinua kichwa chake, lakini
mafundi wamekuja kuzitia hofu na kuzitupa
chini hizi pembe za mataifa ambayo
yaliinua pembe zao dhidi ya nchi ya Yuda
na kuwatawanya watu wake.”

*Maono Ya Tatu: Mtu Mwenye Kamba Ya Kupimia*

2 Kisha nikatazama juu: pale mbele yangu
alikuwepo mtu mwenye kamba ya
kupimia mkononi mwake! [2] [d]Nikamuuliza,
“Unakwenda wapi?”
Akanijibu, “Kupima Yerusalemu, kupata
urefu na upana wake.”
[3] Kisha malaika aliyekuwa akizungumza
nami akaondoka, malaika mwingine akaja
kukutana naye [4] [e]na kumwambia: “Kimbia,
umwambie yule kijana, ‘Yerusalemu
utakuwa mji usio na kuta kwa sababu
ya wingi wa watu na mifugo iliyomo.
[5] [f]Mimi mwenyewe nitakuwa ukuta wa
moto kuuzunguka,’ asema Bwana, ‘nami
nitakuwa utukufu wake ndani yake.’
[6] [g]“Njooni! Njooni! Kimbieni mtoke
katika nchi ya kaskazini,” asema Bwana,
“Kwa kuwa nimewatawanya kwenye pande
nne za mbingu,” asema Bwana.
[7] [h]“Njoo, ee Sayuni! Kimbia, wewe
ukaaye ndani ya Binti Babeli!” [8] [i]Kwa kuwa
hivi ndivyo asemavyo Bwana Mwenye
Nguvu Zote: “Baada ya yeye kuniheshimu
na kunituma mimi dhidi ya mataifa
yaliyokuteka nyara, kwa kuwa yeyote
awagusaye ninyi, anaigusa mboni ya jicho
lake, [9] [j]hakika nitauinua mkono wangu
dhidi yao ili watumwa wao wawateke
nyara. Ndipo mtakapojua ya kwamba
Bwana Mwenye Nguvu Zote amenituma.
[10] [k]“Piga kelele na ufurahie, ee Binti
Sayuni, kwa maana ninakuja, nami
nitaishi miongoni mwenu,” asema Bwana.
[11] [l]“Mataifa mengi yataunganishwa na
Bwana siku hiyo, nao watakuwa watu
wangu. Nitaishi miongoni mwenu nanyi
mtajua kwamba Bwana Mwenye Nguvu
Zote amenituma kwenu. [12] [m]Bwana atairithi
Yuda kama fungu lake katika nchi takatifu
na atachagua tena Yerusalemu. [13] [n]Tulieni
mbele za Bwana, enyi watu wote, kwa
sababu ameinuka kutoka makao yake
matakatifu.”

---

[a]**1:17** Isa 14:1; 40:1; 54:8-10; 61:4; Ezr 9:9; Za 51:18; Isa 51:3; Zek 3:2
[b]**1:19** Amo 6:13; Ezr 4:1; Hab 3:14
[c]**1:21** 1Fal 22:11; Za 75:4, 10; Isa 54:16-17; Zek 12:9
[d]**2:2** Eze 40:3; Zek 1:16; Ufu 21:15
[e]**2:4** Eze 38:11; Isa 49:20; Yer 30:19; 33:22; Zek 14:11; Eze 36:10
[f]**2:5** Isa 10:17; 11:10; 24:23; 26:1; Eze 38:14; 42:20; Za 46:5; 85:9; 125:2; Ufu 21:23; Isa 4:5
[g]**2:6** Za 44:11; Eze 17:21; 37:9; Mt 24:31; Mk 13:27; Kum 28:64
[h]**2:7** Isa 42:7; 48:20; Yer 3:18
[i]**2:8** Kum 32:10; 2The 1:6
[j]**2:9** Isa 14:2; 48:16; Yer 12:14; Hab 2:8; Zek 4:9; 6:15
[k]**2:10** Sef 3:14; Isa 23:12; Kut 25:8; Hes 23:21; Law 26:12; Zek 8:3; 9:9; Ufu 21:3; 2Kor 6:16
[l]**2:11** Yer 23:7; Mik 4:2; Zek 8:8, 20-22; Isa 2:2-3; Kut 12:49; Eze 33:33
[m]**2:12** Kut 34:9; Za 33:12; Yer 10:16; 40:5; Kum 12:5; Isa 14:1; Kum 32:9
[n]**2:13** Kut 14:14; Isa 41:1; Kum 26:15; Za 46:10; Hab 2:20; Rum 3:19

*Maono Ya Nne: Mavazi Safi Kwa Ajili Ya Kuhani Mkuu*

**3** [a]Kisha akanionyesha Yoshua,[b] kuhani mkuu, akiwa amesimama mbele ya malaika wa BWANA, naye Shetani amesimama upande wake wa kuume ili amshtaki. 2 [c]BWANA akamwambia Shetani, "BWANA akukemee Shetani! BWANA, ambaye ameichagua Yerusalemu, akukemee! Je, mtu huyu siyo kijinga kinachowaka kilichonyakuliwa kwenye moto?"

3 [d]Wakati huu, Yoshua alikuwa amevaa nguo chafu alipokuwa amesimama mbele ya malaika. 4 [e]Malaika akawaambia wale waliokuwa wamesimama mbele yake, "Mvueni hizo nguo zake chafu."

Kisha akamwambia Yoshua, "Tazama, nimeiondoa dhambi yako, nami nitakuvika mavazi ya kitajiri."

5 [f]Kisha nikasema, "Mvike kilemba kilicho safi kichwani mwake." Kwa hiyo wakamvika kilemba safi kichwani na kumvika yale mavazi mengine, wakati malaika wa BWANA akiwa amesimama karibu.

6 Malaika wa BWANA akamwamuru Yoshua: 7 [gh]"Hivi ndivyo asemavyo BWANA Mwenye Nguvu Zote: 'Ikiwa utakwenda katika njia zangu na kushika masharti yangu, basi utaitawala nyumba yangu na kuwa na amri juu ya nyua zangu, nami nitakupa nafasi miongoni mwa hawa wasimamao hapa.

8 [i]" 'Sikiliza, ee Yoshua kuhani mkuu, pamoja na wenzako walioketi mbele yako, ambao ni watu walio ishara ya mambo yatakayokuja: Ninakwenda kumleta mtumishi wangu, Tawi. 9 Tazama, jiwe nililoliweka mbele ya Yoshua! Kuna macho saba juu ya jiwe lile moja, nami nitachora maandishi juu yake,' asema BWANA Mwenye Nguvu Zote, 'nami nitaiondoa dhambi ya nchi hii kwa siku moja.

10 [j]" 'Katika siku hiyo kila mmoja wenu atamwalika jirani yake akae chini ya mzabibu wake na mtini wake,' asema BWANA Mwenye Nguvu Zote."

*Maono Ya Tano: Kinara Cha Taa Cha Dhahabu Na Mizeituni Miwili*

**4** [k]Kisha malaika aliyezungumza nami akarudi na kuniamsha, kama mtu aamshwavyo kutoka usingizi wake. 2 [l]Akaniuliza, "Unaona nini?"

Nikajibu, "Ninaona kinara cha taa cha dhahabu tupu, nacho kina bakuli juu yake na taa zake saba juu yake, tena iko mirija saba ya kuleta mafuta, kwenye taa zote zilizo juu yake. 3 [m]Pia kuna mizeituni miwili karibu yake, mmoja upande wa kuume wa bakuli na mwingine upande wa kushoto."

4 Nikamuuliza malaika aliyezungumza nami, "Hivi ni vitu gani, bwana wangu?"

5 [n]Akanijibu, "Hujui kuwa hivi ni vitu gani?"

Nikajibu, "Hapana, bwana wangu."

6 [o]Kisha akaniambia, "Hili ni neno la BWANA kwa Zerubabeli: 'Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa Roho yangu,' asema BWANA Mwenye Nguvu Zote.

7 [p]"Wewe ni kitu gani, ee mlima mkubwa sana? Mbele ya Zerubabeli wewe utakuwa ardhi tambarare. Kisha ataweka jiwe la juu kabisa la mwisho na watu wakipiga kelele wakisema, 'Mungu libariki! Mungu libariki!' "

8 Kisha neno la BWANA likanijia:

---

[a]**3:1** Ezr 2:2; Zek 6:11; 2Sam 24:1; 2Nya 18:21; Za 109:6; Mt 4:10; Ay 1:6; Ufu 12:10
[b]1 Yoshua kwa Kiebrania ni Yeshua, maana yake ni Yehova ni wokovu.
[c]**3:2** Yud 9, 23; Isa 14:1; 7:4; Za 109:31; Mt 4:10; Lk 22:31; Rum 16:20; 8:33; 11:5
[d]**3:3** Isa 64:6
[e]**3:4** 2Sam 12:13; Eze 36:25; Mik 7:18; Mwa 41:42; Za 132:9; Ufu 19:8; Isa 52:1
[f]**3:5** Kut 29:6
[g]**3:7** Law 8:35; Kum 17:8-11
[h]**3:7** Eze 44:15-16; 2Nya 23:6; Yer 15:19; Zek 6:15
[i]**3:8** Kum 28:46; Eze 12:11; Isa 4:2; 49:3
[j]**3:10** Ay 11:18; Hes 16:14; 1Fal 4:25; Mik 4:4
[k]**4:1** Dan 8:18; Yer 31:26
[l]**4:2** Yer 1:13; Kut 25:31; Ufu 1:12; 4:5
[m]**4:3** Ufu 11:4; Za 1:3
[n]**4:5** Zek 1:9
[o]**4:6** 1Nya 3:19; Ezr 5:2; 1Sam 2:9; 13:22; 1Fal 19:12; Neh 9:20; Dan 2:34; Isa 11:2-4
[p]**4:7** Za 26:12; 118:22; Yer 51:25; 1Nya 15:28; Isa 40:3-4; Mt 21:21; Ezr 3:11

9 [a]“Mikono ya Zerubabeli iliweka msingi wa
Hekalu hili, mikono yake pia italimalizia.
Kisha mtajua ya kuwa BWANA Mwenye
Nguvu Zote amenituma mimi kwenu.
10 [b]“Ni nani anayeidharau siku ya mambo
madogo? Watu watashangilia watakapoona
timazi mkononi mwa Zerubabeli.
“(Hizi saba ni macho ya BWANA ambayo
huzunguka duniani kote.)”
11 [c]Kisha nikamuuliza yule malaika, “Hii
mizeituni miwili iliyoko upande wa kuume
na wa kushoto wa kinara cha taa ni nini?”
12 Tena nikamuuliza, “Haya matawi
mawili ya mizeituni karibu na hiyo mirija
miwili ya dhahabu inayomimina mafuta ya
dhahabu ni nini?”
13 Akajibu, “Hujui kuwa haya ni nini?”
Nikamjibu, “Hapana, bwana wangu.”
14 [d]Kwa hiyo akasema, “Hawa ni wawili
ambao wamepakwa mafuta ili kumtumikia
Bwana wa dunia yote.”

*Maono Ya Sita: Kitabu Kinachoruka*

5 [e]Nikatazama tena: na hapo mbele yangu
kulikuwa na kitabu kilichoruka!
2 [f]Akaniuliza, “Unaona nini?”
Nikamjibu, “Naona kitabu kinachoruka
chenye, urefu wa dhiraa ishirini[g] na upana
wa dhiraa kumi.”[h]
3 [i]Akaniambia, “Hii ni laana inayotoka
kwenda juu ya nchi yote, kwa kuwa
kufuatana na yale yaliyoandikwa katika
upande mmoja, kila mwizi atafukuziwa
mbali, pia kufuatana na yaliyo upande wa
pili, kila aapaye kwa uongo atafukuziwa
mbali. 4 [j]BWANA Mwenye Nguvu Zote
asema, ‘Nitaituma hiyo laana, nayo itaingia
katika nyumba ya mwizi na nyumba ya
huyo aapaye kwa uongo kwa Jina langu.
Itabaki katika nyumba yake na kuiharibu,
pamoja na mbao zake na mawe yake.’ ”

*Maono Ya Saba: Mwanamke Ndani Ya Kikapu*

5 [k]Kisha yule malaika aliyekuwa
akizungumza nami akanijia na
kuniambia, “Tazama juu uone ni nini kile
kinachojitokeza.”
6 Nikamuuliza, “Ni kitu gani?”
Akanijibu, “Ni kikapu cha kupimia.”
Kisha akaongeza kusema, “Huu ni uovu
wa watu katika nchi nzima.”
7 Kisha kifuniko kilichotengenezwa kwa
madini ya risasi kilichokuwa kimefunika kile
kikapu, kiliinuliwa na ndani ya kile kikapu
alikuwako mwanamke ameketi! 8 [l]Akasema,
“Huu ni uovu,” tena akamsukumia ndani
ya kikapu na kushindilia kifuniko juu ya
mdomo wa kikapu.
9 [m]Kisha nikatazama juu: na pale mbele
yangu, walikuwepo wanawake wawili,
wakiwa na upepo katika mabawa yao!
Walikuwa na mabawa kama ya korongo,
nao wakainua kile kikapu na kuruka nacho
kati ya mbingu na nchi.
10 Nikamuuliza yule malaika aliyekuwa
akizungumza nami, “Wanakipeleka wapi
hicho kikapu?”
11 [n]Akanijibu, “Wanakipeleka katika nchi
ya Babeli na kujenga nyumba kwa ajili yake.
Itakapokuwa tayari, kikapu kitawekwa pale
mahali pake.”

*Maono Ya Nane: Magari Manne Ya Vita*

6 [o]Nikatazama juu tena: nikaona mbele
yangu magari manne ya vita yakija
kutoka kati ya milima miwili, milima ya
shaba! 2 [p]Gari la kwanza lilivutwa na farasi
wekundu, la pili lilivutwa na farasi weusi,
3 [q]la tatu lilivutwa na farasi weupe na gari
la nne lilivutwa na farasi wa madoadoa ya

[a]**4:9** Ezr 3:11; 6:15; Zek 2:9; 6:12; 1Kor 2:4
[b]**4:10** Hag 2:23; Ezr 5:1; Neh 12:1; Ay 38:5; 2Nya 16:9; Ufu 5:6
[c]**4:11** Ufu 11:4
[d]**4:14** Kut 29:7; 40:15; Za 45:7; Isa 20:3; Dan 9:24-26
[e]**5:1** Za 10:7; Yer 36:4
[f]**5:2** Yer 1:13
[g]2 Dhiraa 20 ni sawa na mita 9.
[h]2 Dhiraa 10 ni sawa mita 4.5.
[i]**5:3** Mal 3:9; Kut 20:15; 20:7; Isa 48:1
[j]**5:4** Zek 8:17; Law 14:34-35; Mit 3:33; Hab 2:9-11; Mal 3:5
[k]**5:5** Mik 6:10
[l]**5:8** Mit 6:11
[m]**5:9** Law 11:19
[n]**5:11** Mwa 10:10; Yer 29:5, 28; Dan 1:2
[o]**6:1** 2Fal 2:12
[p]**6:2** Ufu 6:5; Zek 1:8
[q]**6:3** Ufu 6:2

kijivu, wote wenye nguvu. 4 [a]Nikamuuliza
malaika aliyekuwa akizungumza nami,
“Hawa ni nani bwana wangu?”
5 [b]Malaika akanijibu, “Hizi ni roho nne
za mbinguni zisimamazo mbele ya uwepo
wa Bwana wa dunia yote, zinatoka kwenda
kufanya kazi yake. 6 [c]Gari linalovutwa
na farasi weusi linaelekea katika nchi
ya kaskazini, la farasi weupe linaelekea
magharibi na la farasi wa madoadoa ya
kijivu linaelekea kusini.”
7 [d]Wakati hao farasi wenye nguvu
walipokuwa wakitoka, walikuwa
wakijitahidi kwenda duniani kote. Akasema,
“Nenda duniani kote!” Kwa hiyo wakaenda
duniani kote.
8 [e]Kisha akaniita, “Tazama, wale
wanaokwenda kuelekea nchi ya kaskazini
wamepumzisha Roho yangu katika nchi ya
kaskazini.”

*Taji Kwa Ajili Ya Yoshua*

9 Neno la BWANA likanijia kusema:
10 [f]“Chukua fedha na dhahabu kutoka kwa
watu waliohamishwa, yaani Heldai, Tobia
na Yedaya ambao wamefika kutoka Babeli.
Siku iyo hiyo nenda nyumbani kwa Yosia
mwana wa Sefania. 11 [g]Chukua fedha na
dhahabu utengeneze taji, nawe uiweke
kichwani mwa kuhani mkuu Yoshua,
mwana wa Yehosadaki. 12 [h]Umwambie,
hili ndilo asemalo BWANA Mwenye Nguvu
Zote: ‘Huyu ndiye mtu ambaye jina lake
ni Tawi, naye atachipua kutoka mahali
pake na kujenga Hekalu la BWANA. 13 [i]Ni
yeye atakayejenga Hekalu la BWANA, naye
atavikwa utukufu na ataketi kumiliki katika
kiti cha enzi naye atakuwa kuhani katika
kiti chake cha enzi. Hapo patakuwa amani
kati ya hao wawili.’ 14 [j]Taji itatolewa kwa
Heldai, Tobia, Yedaya na Heni mwana
wa Sefania kama kumbukumbu ndani ya
Hekalu la BWANA. 15 [k]Wale walio mbali sana
watakuja na kusaidia kulijenga Hekalu la
BWANA, nanyi mtajua ya kwamba BWANA
Mwenye Nguvu Zote amenituma kwenu.
Hili litatokea ikiwa mtamtii BWANA Mungu
wenu kwa bidii.”

*Haki Na Rehema, Sio Kufunga*

7 [l]Katika mwaka wa nne wa utawala wa
Mfalme Dario, neno la BWANA lilimjia
Zekaria siku ya nne ya mwezi wa tisa,
mwezi wa Kisleu. 2 [m]Watu wa Betheli
walikuwa wamemtuma Shareza na Regem-
Meleki pamoja na watu wao, kumsihi
BWANA 3 [n]kwa kuwauliza makuhani wa
nyumba ya BWANA Mwenye Nguvu Zote
na manabii, “Je, imempasa kuomboleza
na kufunga katika mwezi wa tano, kama
ambavyo nimekuwa nikifanya kwa miaka
mingi?”
4 Kisha neno la BWANA Mwenye
Nguvu Zote likanijia kusema: 5 [o]“Waulize
watu wote wa nchi na makuhani, ‘Je,
mlipofunga na kuomboleza katika mwezi
wa tano na wa saba kwa miaka sabini
iliyopita, mlifunga kweli kwa ajili yangu?
6 [p]Na mlipokuwa mkila na kunywa, je,
hamkuwa mnasherehekea kwa ajili ya nafsi
zenu? 7 [q]Je, haya sio maneno ya BWANA
aliyosema kupitia manabii waliotangulia,
wakati Yerusalemu pamoja na miji
inayoizunguka ilipokuwa katika hali ya
utulivu na ya mafanikio, wakati Negebu
na Shefala zikiwa zimekaliwa na watu?’ ”

---

[a]**6:4** Zek 5:10
[b]**6:5** Eze 37:9; Mt 24:31; Yos 3:11; Za 68:17; Ebr 1:7; 1:7, 14; Dan 7:10; Lk 1:19
[c]**6:6** Yer 1:14
[d]**6:7** Isa 43:6; Mwa 13:17
[e]**6:8** Mhu 10:4; Eze 5:13; 24:13; Zek 1:10
[f]**6:10** Ezr 2:1; 7:14-16; Yer 28:6
[g]**6:11** Kut 28:36; Za 21:3; 1Nya 6:15; Ezr 2:2; 3:2; Zek 3:1
[h]**6:12** Isa 4:2; Eze 17:22; Ezr 3:8-10; Zek 4:6-9; Isa 9:6; Mik 5:5; Yer 23:5; 33:15; Zek 13:7; Mk 15:39; Lk 1:78; Yn 1:45; Za 80:15-17; Efe 2:20; Ebr 2:9
[i]**6:13** Za 110:4; 21:5
[j]**6:14** Kut 28:12; Mk 14:9
[k]**6:15** Efe 2:13; Isa 60:10; Zek 2:9-11; Isa 58:12; Yer 7:23
[l]**7:1** Ezr 5:1; Neh 1:1
[m]**7:2** Yer 26:19; Zek 8:21; Hag 2:10-14
[n]**7:3** Zek 12:12-14; 2Fal 25:9; Yer 52:12-14; Kum 17:9; Mal 2:7
[o]**7:5** Isa 58:5; 2Fal 25:25; Dan 9:2; Zek 1:12; Mt 6:16; Rum 14:6
[p]**7:6** Isa 43:23
[q]**7:7** Isa 1:11-20; Yer 22:21; 17:26; 44:4-5

8 Neno la BWANA likamjia tena Zekaria: 9 [a]“Hivi ndivyo asemavyo BWANA Mwenye Nguvu Zote: ‘Fanyeni hukumu za haki, onyesheni rehema na huruma ninyi kwa ninyi. 10 [b]Msimwonee mjane wala yatima, mgeni wala maskini. Msiwaziane mabaya mioyoni mwenu ninyi kwa ninyi.’

11 [c]“Lakini wakakataa kusikiliza, wakanipa kisogo kwa ukaidi na kuziba masikio yao. 12 [d]Wakaifanya mioyo yao migumu kama jiwe gumu na hawakuisikiliza sheria au maneno ambayo BWANA Mwenye Nguvu Zote aliyatuma kwa njia ya Roho wake kupitia manabii waliotangulia. Kwa hiyo BWANA Mwenye Nguvu Zote alikasirika sana.

13 [e]“ ‘Wakati nilipoita, hawakusikiliza, kwa hiyo walipoita, sikusikiliza,’ asema BWANA Mwenye Nguvu Zote. 14 [f]‘Niliwatawanya kwa upepo wa kisulisuli miongoni mwa mataifa yote, mahali ambapo walikuwa wageni. Nchi ikaachwa ukiwa nyuma yao kiasi kwamba hakuna aliyeweza kuingia au kutoka. Hivi ndivyo walivyoifanya ile nchi iliyokuwa imependeza kuwa ukiwa.’ ”

### *BWANA Anaahidi Kuibariki Yerusalemu*

8 Neno la BWANA Mwenye Nguvu Zote likanijia tena. 2 [g]Hili ndilo asemalo BWANA Mwenye Nguvu Zote: “Nina wivu sana kwa ajili ya Sayuni, ninawaka wivu kwa ajili yake.”

3 [h]Hili ndilo asemalo BWANA: “Nitarudi Sayuni na kufanya makao Yerusalemu. Kisha Yerusalemu utaitwa mji wa kweli, mlima wa BWANA Mwenye Nguvu Zote utaitwa Mlima Mtakatifu.”

4 [i]Hili ndilo asemalo BWANA Mwenye Nguvu Zote: “Kwa mara nyingine tena wazee wanaume kwa wanawake walioshiba umri wataketi katika barabara za Yerusalemu, kila mmoja akiwa na mkongojo wake mkononi kwa sababu ya umri wake. 5 [j]Barabara za mji zitajaa wavulana na wasichana wanaocheza humo.”

6 [k]Hili ndilo asemalo BWANA Mwenye Nguvu Zote: “Mambo haya yanaweza kuonekana ya ajabu kwa mabaki ya watu wakati huo, lakini yaweza kuwa ya ajabu kwangu?” asema BWANA Mwenye Nguvu Zote.

7 [l]Hili ndilo asemalo BWANA Mwenye Nguvu Zote: “Nitawaokoa watu wangu kutoka nchi za mashariki na magharibi. 8 [m]Nitawarudisha waje kuishi Yerusalemu, watakuwa watu wangu nami nitakuwa mwaminifu na wa haki kwao kama Mungu wao.”

9 [n]Hili ndilo asemalo BWANA Mwenye Nguvu Zote: “Ninyi ambao sasa mnasikia maneno haya yanayozungumzwa na manabii ambao walikuwepo wakati wa kuwekwa kwa msingi wa nyumba ya BWANA Mwenye Nguvu Zote, mikono yenu na iwe na nguvu ili Hekalu liweze kujengwa. 10 [o]Kabla ya wakati huo, hapakuwepo na ujira kwa mtu wala mnyama. Hakuna mtu aliyeweza kufanya shughuli yake kwa usalama kwa sababu ya adui yake, kwa kuwa nilikuwa nimemfanya kila mtu adui wa jirani yake. 11 [p]Lakini sasa sitawatendea mabaki ya watu hawa kama nilivyowatenda zamani,” asema BWANA Mwenye Nguvu Zote.

---

[a]**7:9** Yer 22:3; 42:5; Zek 8:16; Kum 22:1
[b]**7:10** Yer 49:11; Kut 22:21-22; Law 25:17; Isa 1:23; Ay 35:8; Eze 45:9; Mik 6:8
[c]**7:11** Isa 9:9; Yer 32:33; 11:10; 17:23; 8:5; Eze 5:6
[d]**7:12** Yer 5:3; 17:1; 42:21; Eze 11:19; Neh 9:29; Dan 9:12
[e]**7:13** Yer 7:27; 11:11; 14:12; Mit 1:28; Isa 1:15; Mao 3:44; Eze 20:31
[f]**7:14** Kum 4:27; 28:64-67; Law 26:33; Yer 7:34; 23:19; 44:6; Za 44:11; Isa 33:8; Eze 12:19
[g]**8:2** Yoe 2:18; Nah 1:2
[h]**8:3** Zek 1:16; Isa 1:26; 48:1; 52:8; Yoe 3:21; Zek 2:10; Za 15:2; Yer 33:16; Mik 4:1; Za 48:1-2; Yer 31:23
[i]**8:4** Isa 65:20; 1Sam 2:31
[j]**8:5** Yer 30:20; 31:13
[k]**8:6** Za 118:23; 126:1-3; Yer 32:17, 27; Hes 11:23; Ay 42:2; Lk 1:37; Rum 4:21
[l]**8:7** Za 107:3; Isa 11:11; 43:5
[m]**8:8** Eze 11:19-20; 36:28; 37:12; Zek 2:11; 10:10; Yer 11:4; 31:24; Isa 51:16; Ebr 8:10; Law 25:17; Yer 4:2; Zek 4:2; 13:9; Ufu 21:3
[n]**8:9** Ezr 5:1; 3:11; Hag 2:4
[o]**8:10** Isa 5:10; Hag 1:6; 2Nya 15:5
[p]**8:11** Isa 12:1

12 [a]"Mbegu itakua vizuri, mzabibu utazaa
matunda yake, ardhi itatoa mazao yake,
na mbingu zitadondosha umande wake.
Vitu hivi vyote nitawapa mabaki ya watu
kama urithi wao. 13 [b]Jinsi mlivyokuwa kitu
cha laana katikati ya mataifa, ee Yuda na
Israeli, ndivyo nitakavyowaokoa, nanyi
mtakuwa baraka. Msiogope, bali iacheni
mikono yenu iwe na nguvu."

14 [c]Hili ndilo asemalo Bwana Mwenye
Nguvu Zote: "Kama nilivyokuwa
nimekusudia kuleta maangamizi juu
yenu, wakati baba zenu waliponikasirisha
na sikuonyesha huruma," asema Bwana
Mwenye Nguvu Zote, 15 [d]"hivyo sasa
nimeazimia kufanya mema tena kwa
Yerusalemu na Yuda. Msiogope. 16 [e]Haya
ndiyo mtakayoyafanya: Semeni kweli kila
mtu kwa mwenzake, na mtoe hukumu
ya kweli na haki kwenye mahakama
zenu, 17 [f]usipange mabaya dhidi ya jirani
yako, wala msipende kuapa kwa uongo.
Nayachukia yote haya," asema Bwana.

18 Neno la Bwana Mwenye Nguvu Zote
likanijia tena. 19 [g]Hili ndilo asemalo Bwana
Mwenye Nguvu Zote: "Saumu za miezi ya
nne, tano, saba na kumi itakuwa sikukuu
za furaha na za shangwe kwa Yuda. Kwa
hiyo uipende kweli na amani."

20 Hili ndilo asemalo Bwana Mwenye
Nguvu Zote: "Mataifa mengi na wakazi
wa miji mingi watakuja, 21 [h]na wenyeji
wa mji mmoja watakwenda kwenye mji
mwingine na kusema, 'Twende mara moja
na tukamsihi Bwana, na kumtafuta Bwana
Mwenye Nguvu Zote. Mimi mwenyewe
ninakwenda.' 22 [i]Pia watu wa kabila
nyingi na mataifa yenye nguvu yatakuja
Yerusalemu kumtafuta Bwana Mwenye
Nguvu Zote na kumsihi."

23 [j]Hili ndilo asemalo Bwana Mwenye
Nguvu Zote: "Katika siku hizo watu
kumi kutoka lugha zote na mataifa,
watang'ang'ania upindo wa joho la Myahudi
mmoja na kusema, 'Twende pamoja nawe
kwa sababu tumesikia kwamba Mungu yu
pamoja nawe.' "

*Hukumu Juu Ya Adui Za Israeli*

9 Neno:

[k]Neno la Bwana liko
kinyume na nchi ya Hadraki
na Dameski itakuwa mahali pa
kupumzika,
kwa kuwa macho ya watu na ya
kabila zote
za Israeli yako kwa Bwana,
2 [l]pia juu ya Hamathi inayopakana
nayo,
juu ya Tiro na Sidoni,
ingawa wana ujuzi mwingi sana.
3 [m]Tiro amejijengea ngome imara,
amelundika fedha kama mavumbi
na dhahabu kama taka za mitaani.
4 [n]Lakini Bwana atamwondolea mali
zake
na kuuangamiza uwezo wake wa
baharini,
naye atateketezwa kwa moto.
5 [o]Ashkeloni ataona hili na kuogopa;
Gaza atagaagaa kwa maumivu
makali,
pia Ekroni, kwa sababu
matumaini yake yatanyauka.

---

[a]**8:12** Za 65:13; 85:12; Yoe 2:22; Za 67:6; Mwa 27:28; Isa 60:21; Hos 2:21; Oba 1:17; Isa 61:7; Mt 6:33; 1Tim 4:8
[b]**8:13** Hes 5:27; Kum 13:15; Yer 42:18; Za 102:8; 48:8; Mwa 12:2; Yoe 2:14; Hag 2:5; Efe 6:10
[c]**8:14** Eze 24:14; Yer 31:28; 2Nya 36:16
[d]**8:15** Yer 29:11; 31:28; 32:42; Mik 7:18-20
[e]**8:16** Za 15:2; Yer 33:16; Eze 18:8; 45:9; Amo 5:15; Zek 7:9; Efe 4:25; Mit 12:19
[f]**8:17** Mit 3:29; 6:16-19; Yer 7:9; Zek 5:4
[g]**8:19** 2Fal 25:7, 25; Yer 39:2; 52:4, 12; Za 30:11; Yer 41:1; Isa 35:10
[h]**8:21** Zek 7:2; Yer 26:19
[i]**8:22** Za 86:9; 117:1; Isa 2:2-3; 44:5; 45:14; 49:6; Zek 2:11
[j]**8:23** Za 102:22; Isa 13:1; 14:1; 45:14; 56:3; 1Kor 14:25; Yer 23:33
[k]**9:1** Isa 17:1; Amo 1:5; Za 145:15
[l]**9:2** Yer 49:23; Eze 28:1-19; Mwa 10:15; Amo 1:9; Oba 1:20
[m]**9:3** Ay 27:16; Eze 28:4
[n]**9:4** Isa 23:1, 11; Yer 25:22; Eze 26:3-5; 27:32-36; 28:18
[o]**9:5** Yer 47:5; Sef 2:5; Mdo 8:26

Gaza atampoteza mfalme wake
na Ashkeloni ataachwa pweke.
6 [a]Wageni watakalia mji wa Ashdodi,
nami nitakatilia mbali kiburi cha Wafilisti.
7 [b]Nitaondoa damu vinywani mwao,
chakula kile walichokatazwa kati ya meno yao.
Mabaki yao yatakuwa mali ya Mungu wetu,
nao watakuwa viongozi katika Yuda,
naye Ekroni atakuwa kama Wayebusi.
8 [c]Lakini nitailinda nyumba yangu
dhidi ya majeshi ya wanyang'anyi.
Kamwe mdhalimu hatashambulia watu wangu tena,
kwa maana sasa ninawachunga.

### *Kuja Kwa Mfalme Wa Sayuni*

9 [d]Shangilia sana, ee Binti Sayuni!
Piga kelele, Binti Yerusalemu!
Tazama, Mfalme wako anakuja kwako,
ni mwenye haki, naye ana wokovu,
ni mpole, naye amepanda punda,
mwana-punda, mtoto wa punda.
10 [e]Nitaondoa magari ya vita kutoka Efraimu
na farasi wa vita kutoka Yerusalemu,
nao upinde wa vita utavunjwa.
Atatangaza amani kwa mataifa.
Utawala wake utaenea kutoka bahari hadi bahari,
na kutoka Mto Frati hadi mwisho wa dunia.
11 [f]Kwako wewe, kwa sababu ya damu ya Agano langu nawe,
nitawaacha huru wafungwa wako
watoke kwenye shimo lisilo na maji.
12 [g]Rudieni ngome yenu, enyi wafungwa wa tumaini;
hata sasa ninatangaza kwamba
nitawarejesheeni maradufu.
13 [h]Nitampinda Yuda kama nipindavyo upinde wangu,
nitamfanya Efraimu mshale wangu.
Nitawainua wana wako, ee Sayuni,
dhidi ya wana wako, ee Uyunani,
na kukufanya kama upanga wa shujaa wa vita.

### *Bwana Atatokea*

14 Kisha Bwana atawatokea;
mshale wake utamulika
kama umeme wa radi.
Bwana Mwenyezi atapiga tarumbeta,
naye atatembea katika tufani za kusini,
15 [i]na Bwana Mwenye Nguvu Zote atawalinda.
Wataangamiza na kushinda
kwa mawe ya kutupa kwa kombeo.
Watakunywa na kunguruma kama waliolewa mvinyo;
watajaa kama bakuli linalotumika kunyunyizia
kwenye pembe za madhabahu.
16 [j]Bwana Mungu wao atawaokoa siku hiyo
kama kundi la watu wake.

---

[a]**9:6** Isa 14:30
[b]**9:7** Ay 25:2; Yoe 3:4; Sef 2:4; Yer 47:1
[c]**9:8** Isa 26:1; 52:1; 54:14; Zek 14:21; Yoe 3:17; Kum 33:27; Za 34:7; Kut 3:7
[d]**9:9** Isa 62:11; 9:6-7; 43:3-11; 1Fal 1:39; Za 24:7; 149:2; Mik 4:8; Yer 23:5-6; Sef 3:14-15; Zek 2:10; Mwa 49:11; Mt 21:5; 1Fal 1:33; Yn 12:15; 1:49; Lk 19:38; Mdo 22:14; 1Pet 3:18
[e]**9:10** Mik 4:3; 5:10; Hos 1:7; 2:18; Zek 10:4; Isa 2:4; Za 72:8; Isa 11:10; Efe 2:14; Kol 1:20-21; Za 2:8; Isa 9:6-7; Mik 5:4; Ufu 11:15
[f]**9:11** Kut 24:8; Mt 26:28; Lk 22:20; Isa 10:4; 42:7; Yer 38:6; Isa 61:1
[g]**9:12** Yoe 3:16; Isa 40:2; Kum 21:17
[h]**9:13** 2Sam 22:25; Isa 49:2; Yoe 3:6; Yer 51:20
[i]**9:15** Isa 31:5; 37:35; Zek 12:8; 10:7; 14:3, 20; Kut 27:2; Law 4:25
[j]**9:16** Isa 10:20; Yer 31:11; Eze 37:23; Mal 3:17; Isa 11:12

Watang'ara katika nchi yake
kama vito vya thamani kwenye taji.
17 Jinsi gani watavutia na kuwa wazuri!
Nafaka itawastawisha vijana wanaume,
nayo divai mpya vijana wanawake.

*Bwana Ataitunza Yuda*

10 [a]Mwombeni Bwana mvua wakati wa vuli;
ndiye Bwana atengenezaye mawingu ya tufani.
Huwapa watu manyunyu ya mvua,
pia mimea ya shambani kwa ajili ya kila mtu.
2 [b]Sanamu huzungumza udanganyifu,
waaguzi huona maono ya uongo;
husimulia ndoto ambazo si za kweli,
wanatoa faraja batili.
Kwa hiyo watu wanatangatanga kama kondoo
walioonewa kwa kukosa mchungaji.

3 [c]"Hasira yangu inawaka dhidi ya wachungaji,
nami nitawaadhibu viongozi;
kwa kuwa Bwana Mwenye Nguvu Zote
atalichunga kundi lake,
nyumba ya Yuda,
naye atawafanya kuwa kama farasi
mwenye kiburi akiwa vitani.
4 [d]Kutoka Yuda litatokea Jiwe la pembeni,
kutoka kwake vitatoka vigingi vya hema,
kutoka kwake utatoka upinde wa vita,
kutoka kwake atatoka kila mtawala.
5 [e]Kwa pamoja watakuwa kama mashujaa
wanaokanyaga barabara za matope
wakati wa vita.
Kwa sababu Bwana yu pamoja nao,
watapigana na kuwashinda wapanda farasi.

6 [f]"Nitaiimarisha nyumba ya Yuda
na kuiokoa nyumba ya Yosefu.
Nitawarejesha kwa sababu
nina huruma juu yao.
Watakuwa kama watu ambao
sijawahi kuwakataa
kwa sababu mimi ndimi Bwana Mungu wao,
nami nitawajibu.
7 [g]Waefraimu watakuwa kama mashujaa,
mioyo yao itafurahi kana kwamba ni kwa divai.
Watoto wao wataona na kufurahi,
mioyo yao itashangilia katika Bwana.
8 [h]Nitawaashiria na kuwakusanya ndani.
Hakika nitawakomboa,
nao watakuwa wengi
kama walivyokuwa mwanzoni.

---

[a]**10:1** Law 26:4; 1Fal 8:36; Za 104:13; 135:7; Ay 14:9; Yer 14:22; Yoe 2:32
[b]**10:2** Eze 21:21; Isa 44:25; 40:19; Yer 23:16; Hes 27:17; Hos 3:4; Mt 9:36
[c]**10:3** Isa 14:9; Yer 25:34; Eze 34:8-10; Kut 4:31; Rut 1:6; Sef 2:7; Lk 1:68; 1Pet 2:12
[d]**10:4** Za 118:22; Mdo 4:11; Isa 22:23; Zek 9:10
[e]**10:5** 2Sam 22:43; Mik 7:10; 5:8; Amo 2:15; Hag 2:22; Zek 12:4
[f]**10:6** Eze 30:24; 36:37; Za 102:13; 34:17; Isa 37:19; 14:1; 58:9; 65:24; Zek 8:7-8; 13:9
[g]**10:7** Zek 9:15; 1Sam 2:1; Isa 60:5; Yoe 2:23
[h]**10:8** Isa 5:26; Yer 33:22; Eze 36:11

[9] [a]Ijapokuwa niliwatawanya miongoni mwa mataifa,
hata hivyo wakiwa katika nchi za mbali
watanikumbuka mimi.
Wao na watoto wao watanusurika katika hatari
nao watarudi.
[10] [b]Nitawarudisha kutoka Misri
na kuwakusanya toka Ashuru.
Nitawaleta katika nchi ya Gileadi na Lebanoni,
na hapo hapatakuwa na nafasi ya kuwatosha.
[11] [c]Watapita katika bahari ya mateso;
bahari iliyochafuka itatulizwa
na vilindi vyote vya Mto Naili vitakauka.
Kiburi cha Ashuru kitashushwa,
nayo fimbo ya utawala ya Misri itatoweka.
[12] [d]Nitawaimarisha katika BWANA,
na katika jina lake watatembea,"
asema BWANA.

11 [1] [e]Fungua milango yako, ee Lebanoni,
ili moto uteketeze mierezi yako!
[2] [f]Piga yowe, ee mti wa msunobari,
kwa kuwa mwerezi umeanguka;
miti ya fahari imeharibiwa!
Piga yowe, enyi mialoni ya Bashani,
msitu mnene umefyekwa!
[3] [g]Sikiliza yowe la wachungaji;
malisho yao manono yameangamizwa!
Sikia ngurumo za simba;
kichaka kilichostawi sana
cha Yordani kimeharibiwa!

*Wachungaji Wawili Wa Kondoo*

[4] [h]Hili ndilo asemalo BWANA Mungu
wangu: "Lilishe kundi lililokusudiwa
kuchinjwa. [5] [i]Wanunuzi wake huwachinja
na kuondoka pasipo kuadhibiwa.
Wale wanaowauza husema, 'BWANA
asifiwe, mimi ni tajiri!' Wachungaji wao
wenyewe hawawahurumii. [6] [j]Kwa kuwa
sitawahurumia tena watu wa nchi,"
asema BWANA. "Nitawakabidhi kila mtu
mkononi mwa jirani yake na mfalme wake.
Wataitenda jeuri nchi, nami sitawaokoa
kutoka mikononi mwao."

[7] [k]Kwa hiyo nikalilisha kundi lililotiwa
alama kwa kuchinjwa, hasa kundi
lililoonewa sana. Kisha nikachukua fimbo
mbili, moja nikaiita Fadhili na nyingine
Umoja, nami nikalilisha kundi. [8] [l]Katika
mwezi mmoja nikawaondoa wachungaji
watatu.

Kundi la kondoo likanichukia, nami
nikachoshwa nao, [9] [m]nikasema, "Sitakuwa
mchungaji wenu. Waache wanaokufa
wafe na wanaoangamia waangamie. Wale
waliobakia kila mmoja na ale nyama ya
mwenzake."

[10] [n]Kisha nikachukua fimbo yangu
inayoitwa Fadhili nikaivunja, kutangua
Agano nililofanya na mataifa yote.
[11] Likatanguka siku hiyo, kwa hiyo wale
waliodhurika katika kundi, waliokuwa
wakiniangalia wakajua kuwa hilo lilikuwa
neno la BWANA.

[12] [o]Nikawaambia, "Mkiona kuwa ni
vyema, nipeni ujira wangu, la sivyo, basi
msinipe." Kwa hiyo wakanilipa vipande
thelathini vya fedha.

[13] [p]Naye BWANA akaniambia,
"Mtupie mfinyanzi," hiyo bei nzuri
waliyonithaminia! Kwa hiyo nikachukua

[a]**10:9** Isa 44:21; Eze 6:9
[b]**10:10** Isa 11:11; 49:19; Zek 8:8; Yer 50:19; Rum 11:25; Kut 14:26-27
[c]**10:11** Isa 19:5-7; 51:10; Sef 2:13; Eze 29:15; 30:13
[d]**10:12** Eze 30:24; Mik 4:5
[e]**11:1** Eze 31:3; 2Nya 36:19; Zek 12:6
[f]**11:2** Isa 2:13; 32:19; 10:34
[g]**11:3** Isa 5:29; Yer 2:15; 50:44; Eze 19:9
[h]**11:4** Yer 25:34
[i]**11:5** Yer 50:7; Eze 34:2-3; Kum 29:19; Yer 2:3; Hos 12:8; Yn 16:2; 1Tim 6:9; 2Pet 2:3
[j]**11:6** Zek 14:13; Isa 9:19-21; Yer 13:14; Mao 2:21; 5:8; Mik 5:8; 7:2-6
[k]**11:7** Yer 25:34; Sef 3:12; Mt 11:5
[l]**11:8** Eze 14:5; Hos 5:7
[m]**11:9** Yer 43:11; 15:2; Isa 9:20
[n]**11:10** Za 89:39; Yer 14:21
[o]**11:12** Mwa 23:16; Mt 26:15; Kut 21:32
[p]**11:13** Kut 21:32; Mt 27:9-10; Mdo 1:18-19

hivyo vipande thelathini vya fedha na
kumtupia huyo mfinyanzi katika nyumba
ya BWANA.
14 Kisha nikaivunja fimbo yangu ya pili
iitwayo Umoja, kuvunja undugu kati ya
Yuda na Israeli!
15 Kisha BWANA akaniambia, “Vitwae
tena vifaa vya mchungaji mpumbavu.
16 Kwa maana ninakwenda kumwinua
mchungaji juu ya nchi ambaye hatamjali
aliyepotea, wala kuwatafuta wale
wachanga au kuwaponya waliojeruhiwa,
wala kuwalisha wenye afya, lakini atakula
nyama ya kondoo wanono na kuzirarua
kwato zao.

17 [a]“Ole wa mchungaji asiyefaa,
anayeliacha kundi!
Upanga na uupige mkono wake na
jicho lake la kuume!
Mkono wake na unyauke kabisa,
jicho lake la kuume lipofuke
kabisa!”

*Maadui Wa Yerusalemu Kuangamizwa*

12 [b]Hili ni neno la BWANA kuhusu Israeli.
BWANA, yeye azitandaye mbingu,
awekaye misingi ya dunia na aiumbaye
roho ya mwanadamu ndani yake, asema:
2 [c]“Nitakwenda kufanya Yerusalemu
kuwa kikombe cha kuyumbisha mataifa
yote yanayoizunguka. Yuda utazingirwa
kwa vita na Yerusalemu pia. 3 [d]Katika
siku hiyo, wakati mataifa yote ya dunia
yatakapokusanyika dhidi yake, nitaufanya
Yerusalemu kuwa jabali lisilosogezwa
kwa mataifa yote. Wote watakaojaribu
kulisogeza watajiumiza wenyewe. 4 [e]Katika
siku hiyo nitampiga kila farasi kwa hofu ya
ghafula, naye ampandaye nitampiga kwa
uwazimu,” asema BWANA. “Nitalielekeza
jicho langu la ulinzi juu ya nyumba ya Yuda,
nami nitawapofusha farasi wote wa mataifa.
5 [f]Kisha viongozi wa Yuda watasema
mioyoni mwao, ‘Watu wa Yerusalemu wana
nguvu kwa sababu BWANA Mwenye Nguvu
Zote ni Mungu wao.’
6 [g]“Katika siku hiyo nitawafanya viongozi
wa Yuda kuwa kama kigae cha moto ndani
ya lundo la kuni, kama mwenge uwakao
kati ya miganda. Watateketeza kulia na
kushoto mataifa yote yanayowazunguka,
lakini Yerusalemu utabaki salama mahali
pake.
7 [h]“BWANA atayaokoa makao ya Yuda
kwanza, ili heshima ya nyumba ya Daudi na
wakazi wa Yerusalemu isiwe kubwa zaidi
kuliko ile ya Yuda. 8 [i]Katika siku hiyo, BWANA
atawakinga wale waishio Yerusalemu, ili
kwamba aliye dhaifu kupita wote miongoni
mwao awe kama Daudi, nayo nyumba ya
Daudi itakuwa kama Mungu, kama Malaika
wa BWANA akiwatangulia. 9 [j]Katika siku
hiyo nitatoka kuangamiza mataifa yote
yatakayoshambulia Yerusalemu.

*Kumwombolezea Yule Aliyechomwa Mkuki*

10 [k]“Nami nitamiminia nyumba ya Daudi
na wakazi wa Yerusalemu roho ya neema[l]
na maombi. Watanitazama mimi, yule
waliyemchoma. Nao watamwombolezea
kama mtu anayemwombolezea mwanawe
wa pekee na kusikitika kwa uchungu
kama anayemsikitikia mzaliwa wake wa
kwanza wa kiume. 11 [m]Katika siku hiyo
kilio kitakuwa kikubwa Yerusalemu, kama
kilio cha Hadad-Rimoni katika tambarare
ya Megido. 12 [n]Nchi itaomboleza, kila ukoo
peke yake, nao wake zao peke yao. Ukoo
wa nyumba ya Daudi na wake zao, ukoo wa
nyumba ya Nathani na wake zao, 13 ukoo

[a]**11:17** Yer 23:1; Eze 30:21-22; Isa 13:1; Yn 10:12; Mik 3:6
[b]**12:1** Mwa 1:8; Za 102:25; 104:2; Yer 51:15; Ebr 1:10; Isa 57:16; Ebr 12:9
[c]**12:2** Za 78:5; 60:3; Isa 51:23; Zek 14:14
[d]**12:3** Isa 28:16; 29:8; 66:18; Zek 14:2; Dan 2:34-35; Mt 21:44
[e]**12:4** Za 76:6; Zek 10:5
[f]**12:5** Eze 30:24
[g]**12:6** Isa 10:17-18; Zek 11:1; 14:10; Oba 1:18
[h]**12:7** Yer 30:18; Amo 9:11
[i]**12:8** Za 91:4; 82:6; Yoe 3:10, 16; Zek 9:15; Mik 7:8
[j]**12:9** Isa 29:7; Zek 1:21; 14:2-3; 1Kor 1:27-31
[k]**12:10** Eze 37:9; 39:29; Isa 44:3; Yoe 2:28-29; Za 22:16; Yn 19:34-37; Amu 11:34; Mwa 21:16; Yer 31:19; Yoe 2:28; Lk 2:35; Ufu 1:7
[l]10 Au: Roho wa neema.
[m]**12:11** Yer 50:4; 2Fal 23:29; Mdo 2:37; 2Nya 35:24
[n]**12:12** Mt 24:30; Ufu 1:7

wa nyumba ya Lawi na wake zao, ukoo
wa Shimei na wake zao, 14 [a]na koo zote
zilizobaki na wake zao.

*Kutakaswa Dhambi*

13 [b]“Katika siku hiyo, chemchemi
itafunguliwa kwa nyumba ya Daudi
na wakazi wa Yerusalemu, kuwatakasa
dhambi na unajisi.
2 [c]“Katika siku hiyo, nitayakatilia mbali
majina ya sanamu kutoka nchi, nayo
hayatakumbukwa tena,” asema BWANA
Mwenye Nguvu Zote. “Nitaondoa manabii
wao pamoja na roho ya uchafu katika
nchi. 3 [d]Ikiwa yupo yeyote atakayeendelea
kutabiri, baba yake na mama yake
waliomzaa watamwambia, ‘Ni lazima ufe,
kwa sababu umesema uongo kwa jina
la BWANA.’ Atakapotabiri, wazazi wake
mwenyewe watampasua tumbo.
4 [e]“Katika siku hiyo, kila nabii ataaibika
kwa maono ya unabii wake. Hatavaa vazi
la kinabii la nywele ili apate kudanganya
watu. 5 [f]Atasema, ‘Mimi sio nabii. Mimi ni
mkulima; ardhi imekuwa kazi yangu tangu
ujana wangu.’ 6 Ikiwa mtu atamuuliza,
‘Majeraha haya yaliyo mwilini mwako ni
ya nini?’ Atajibu, ‘Ni majeraha niliyoyapata
katika nyumba ya rafiki zangu.’

*Mchungaji Apigwa, Nao Kondoo Watawanyika*

7 [g]“Amka, ee upanga, dhidi ya
mchungaji wangu,
dhidi ya mtu aliye karibu nami!”
asema BWANA Mwenye Nguvu
Zote.
“Mpige mchungaji,
nao kondoo watatawanyika,
nami nitageuza mkono wangu
dhidi ya walio wadogo,
8 [h]katika nchi yote,” asema BWANA,
“theluthi mbili watapigwa na
kuangamia;
hata hivyo theluthi moja watabaki
ndani yake.
9 [i]Hii theluthi moja nitaileta katika
moto;
nitawasafisha kama fedha
isafishwavyo
na kuwajaribu kama dhahabu.
Wataliitia Jina langu
nami nitawajibu;
nitasema, ‘Hawa ni watu wangu,’
nao watasema, ‘BWANA ni Mungu
wetu.’ ”

*BWANA Yuaja Kutawala*

14 [j]Siku ya BWANA inakuja ambayo nyara
zilizotekwa kwenu zitagawanywa
miongoni mwenu.
2 [k]Nitayakusanya mataifa yote huko
Yerusalemu kupigana dhidi yake, mji
utatekwa, nyumba zitavamiwa na kuporwa
na wanawake watanajisiwa. Nusu ya
mji watakwenda uhamishoni, lakini
watakaobaki hawataondolewa kutoka
mjini.
3 [l]Kisha BWANA atatoka na kupigana

[a]**12:14** Zek 7:3
[b]**13:1** Yer 17:13; Law 16:30; Za 51:2; Ebr 9:14; Isa 1:16-17; Yn 1:29; 1Kor 6:11; 1Pet 1:19; 1Yn 1:7
[c]**13:2** Yer 43:12; 23:14-15; Eze 6:6; 36:25; Hos 2:17; Mik 5:13; 1Fal 22:22; Kut 23:13; 2Pet 2:1
[d]**13:3** Yer 28:16; 23:34; Kum 13:6-11; 18:20; Neh 6:14; Eze 14:9
[e]**13:4** Yer 6:15; Mt 3:5; 1Fal 18:7; Isa 20:2; Eze 12:24; Mik 3:6-7
[f]**13:5** Amo 7:14
[g]**13:7** Isa 34:5; 40:11; 53:4; Yer 47:6; Eze 37:24; 2Sam 17:2; Mk 4:27; Ebr 13:20; Yn 10:20; 1:29; Mk 14:27
[h]**13:8** Eze 5:2-4, 12; Zek 14:2; Rum 11:5
[i]**13:9** Isa 4:4; 33:14; 30:16; 44:5; Mal 3:2; Za 12:6; 50:15; 86:7; Dan 11:35; 1Pet 1:6-7; Ay 6:29; Yer 6:27; 29:12; 30:22; Law 26:16; Eze 20:38; Isa 48:10; Za 66:10
[j]**14:1** Isa 13:6; 23:18; Yoe 1:15; Mal 4:1
[k]**14:2** Isa 2:3; Zek 12:3; 13:8; Eze 5:8; Mwa 34:29; Mao 5:11; Isa 13:6; Yoe 3:2
[l]**14:3** Zek 9:14-15; 8:9; Isa 8:9

dhidi ya watu wa yale mataifa, kama
apiganavyo siku ya vita. 4 [a]Siku hiyo miguu
yake itasimama juu ya Mlima wa Mizeituni,
mashariki mwa Yerusalemu, nao Mlima wa
Mizeituni utagawanyika mara mbili kuanzia
mashariki hadi magharibi, ukifanya bonde
kubwa, nusu ya mlima ukisogea kuelekea
kaskazini na nusu kuelekea kusini. 5 [b]Nanyi
mtakimbia kupitia katika bonde hilo la
mlima wangu kwa kuwa litaenea hadi Aseli.
Mtakimbia kama mlivyokimbia tetemeko la
ardhi katika siku za Uzia mfalme wa Yuda.
Kisha BWANA Mungu wangu atakuja na
watakatifu wote pamoja naye.

6 [c]Siku hiyo hakutakuwepo nuru, baridi
wala theluji. 7 [d]Itakuwa siku ya kipekee,
isiyo na mchana wala usiku, siku ijulikanayo
na BWANA. Jioni inapofika nuru itakuwepo.

8 [e]Siku hiyo, maji yaliyo hai yatatiririka
kutoka Yerusalemu, nusu kwenda kwenye
bahari ya mashariki,[f] na nusu kwenda
kwenye bahari ya magharibi[g] wakati wa
kiangazi na wakati wa masika.

9 [h]BWANA atakuwa mfalme juu ya dunia
yote. Katika siku hiyo atakuwepo BWANA
mmoja na jina lake litakuwa jina pekee.

10 [i]Nchi yote kuanzia Geba, kaskazini
mwa Yuda, hadi Rimoni, kusini mwa
Yerusalemu, itakuwa kama Araba.[j] Lakini
Yerusalemu utainuliwa juu na kubaki
mahali pake, toka Lango la Benyamini
hadi mahali pa Lango la Kwanza, mpaka
kwenye Lango la Pembeni na kutoka Mnara
wa Hananeli hadi kwenye mashinikizo ya
divai ya mfalme. 11 [k]Utakaliwa na watu,
kamwe hautaharibiwa tena, Yerusalemu
utakaa salama.

12 [l]Hii ndiyo tauni ambayo BWANA atapiga
nayo mataifa yote ambayo yalipigana dhidi
ya Yerusalemu: Nyama ya miili yao itaoza
wangali wamesimama kwa miguu yao,
macho yao yataoza kwenye matundu yake na
ndimi zao zitaoza vinywani mwao. 13 [m]Katika
siku hiyo BWANA atawatia wanaume hofu
kuu. Kila mwanaume atakamata mkono wa
mwenzake nao watashambuliana. 14 [n]Yuda
pia atapigana katika Yerusalemu. Utajiri wa
mataifa yote yanayoizunguka Yerusalemu
utakusanywa, wingi wa dhahabu, fedha
na nguo. 15 Tauni ya aina iyo hiyo itapiga
farasi na nyumbu, ngamia na punda, nao
wanyama wote walioko kwenye kambi za
adui.

16 [o]Kisha walionusurika katika mataifa
yote ambayo yaliushambulia Yerusalemu
watakuwa wakipanda Yerusalemu kila
mwaka kumwabudu Mfalme, BWANA
Mwenye Nguvu Zote na kuadhimisha
Sikukuu ya Vibanda. 17 [p]Ikiwa taifa lolote
la dunia hawatakwenda Yerusalemu
kumwabudu Mfalme, BWANA Mwenye
Nguvu Zote, mvua haitanyesha kwao.
18 [q]Ikiwa watu wa Misri nao hawatakwenda
kushiriki, hawatapata mvua. BWANA ataleta
juu yao tauni ile ambayo itawapiga mataifa
yale ambayo hayatakwenda kuadhimisha
Sikukuu ya Vibanda. 19 [r]Hii itakuwa adhabu
ya Misri na adhabu ya mataifa yote yale
ambayo hayatakwenda Yerusalemu
kuadhimisha Sikukuu ya Vibanda.

---

[a]**14:4** Eze 11:23; Hes 16:31; Mdo 1:11-12; Yoe 3:12
[b]**14:5** Isa 29:6; 66:15-16; Mt 16:27; 25:31; Yud 14; Mt 24:30; Yoe 3:11
[c]**14:6** Isa 13:10; Yer 4:23
[d]**14:7** Yer 30:7; Ufu 21:23-25; 22:5; Isa 13:10; 30:26
[e]**14:8** Eze 47:1-12; Yn 7:38; Ufu 22:1-2; Isa 30:25; Yoe 2:20; Mwa 8:22
[f]8 Yaani Bahari ya Chumvi au Bahari Mfu.
[g]8 Yaani Bahari ya Mediterania.
[h]**14:9** Za 22:28; 47:7; Oba 1:21; Kum 6:4; Isa 45:24; Ufu 15:1; Hab 2:14; Efe 4:5-6; Za 2:8
[i]**14:10** 1Fal 15:22; Yos 15:32; Isa 2:2; Yer 20:2; 30:18; Amo 9:11; Zek 12:6; 2Fal 14:13; Neh 3:1
[j]10 Araba maana yake Nchi tambarare.
[k]**14:11** Zek 2:4; Za 48:8; Eze 34:25-28; Yer 31:40
[l]**14:12** Isa 11:4; Law 26:16; Kum 28:22; Ay 18:13
[m]**14:13** Mwa 35:5; Amu 7:22; Zek 11:6; 1Sam 14:15
[n]**14:14** Zek 12:2; Isa 23:18
[o]**14:16** 2Fal 19:31; Za 22:29; 86:9; Isa 19:21; 60:6-9; Oba 1:21; Kut 23:16; Isa 66:23; 1Tim 6:15; Law 23:34; Neh 8:14; Hos 12:9
[p]**14:17** 2Nya 32:23; Yer 14:4; Amo 4:7; Isa 60:12
[q]**14:18** Mwa 27:29
[r]**14:19** Ezr 3:4

20 [a]Katika siku hiyo, kengele zilizofungwa
kwenye farasi zitaandikwa maneno haya:
TAKATIFU KWA BWANA, navyo vyungu vya
kupikia katika nyumba ya BWANA vitakuwa
kama bakuli takatifu mbele ya madhabahu.
21 [b]Kila chungu kilichoko Yerusalemu na
Yuda kitakuwa kitakatifu kwa BWANA
Mwenye Nguvu Zote na wote wanaokuja
kutoa dhabihu watachukua baadhi ya
vyungu hivyo na kupikia. Katika siku hiyo
hatakuwepo tena mfanyabiashara katika
nyumba ya BWANA Mwenye Nguvu Zote.

---

[a]**14:20** Kut 39:30; Eze 46:20; Zek 9:15
[b]**14:21** Yer 31:40; Rum 14:6-7; 1Kor 10:31; Neh 8:10; 11:1; Eze 44:9; Kol 3:17; Isa 35:8; Ufu 21:27; Efe 2:19

# MALAKI

1 [a]Ujumbe: Neno la BWANA kwa Israeli
kupitia kwa Malaki.

### *Yakobo Alipendwa, Esau Alichukiwa*

[2] [b]BWANA asema, “Nimewapenda ninyi.”
“Lakini ninyi mnauliza, ‘Wewe
umetupendaje?’ ”
BWANA asema, “Je, Esau hakuwa ndugu
yake Yakobo? Hata hivyo nimempenda
Yakobo, [3] [c]lakini nikamchukia Esau, nami
nimeifanya milima yake kuwa ukiwa,
na urithi wake nimewapa mbweha wa
jangwani.”
[4] [d]Edomu anaweza kusema, “Ingawa
tumepondapondwa, tutajenga upya
magofu.”
Lakini hili ndilo BWANA Mwenye Nguvu
Zote asemalo: “Wanaweza kujenga, lakini
nitabomoa. Wataitwa Nchi Ovu, watu
ambao siku zote wapo chini ya ghadhabu
ya BWANA. [5] [e]Mtayaona kwa macho yenu
wenyewe na kusema, ‘BWANA ni mkuu,
hata nje ya mipaka ya Israeli!’

### *Dhabihu Zilizo Na Mawaa*

[6] [f]“Mwana humheshimu baba yake,
naye mtumishi humheshimu bwana wake.
Kama mimi ni baba, iko wapi heshima
ninayostahili? Kama mimi ni bwana,
iko wapi heshima ninayostahili?” asema
BWANA Mwenye Nguvu Zote. “Ni ninyi,
enyi makuhani, mnaolidharau Jina langu.
“Lakini mnauliza, ‘Tumelidharau Jina
lako kwa namna gani?’
[7] [g]“Mnatoa sadaka chakula kilichotiwa
unajisi juu ya madhabahu yangu.
“Lakini ninyi mnauliza, ‘Tumekutia
unajisi kwa namna gani?’
“Kwa kusema kuwa meza ya BWANA
ni ya kudharauliwa. [8] [h]Wakati mletapo
dhabihu za wanyama walio vipofu, je, hilo
si kosa? Mnapoleta dhabihu zilizo vilema
au wanyama wagonjwa, je, hilo si kosa?
Jaribuni kuvitoa kwa mtawala wenu! Je,
angefurahishwa nanyi? Je, atawakubalia?”
asema BWANA Mwenye Nguvu Zote.
[9] [i]“Basi mwombeni Mungu awe na neema
kwetu. Je, kwa sadaka kama hizo kutoka
mikononi mwenu, atawapokea?” asema
BWANA Mwenye Nguvu Zote.
[10] [j]“Laiti mmoja wenu angalifunga
milango ya Hekalu, ili msije mkawasha
moto usiokuwa na faida juu ya madhabahu
yangu! Sina furaha nanyi,” asema BWANA
Mwenye Nguvu Zote, “nami sitaikubali
sadaka toka mikononi mwenu. [11] [k]Jina
langu litakuwa kuu miongoni mwa mataifa,
kuanzia mawio ya jua hata machweo yake.
Kila mahali uvumba na sadaka safi zitaletwa
kwa Jina langu, kwa sababu Jina langu
litakuwa kuu miongoni mwa mataifa,”
asema BWANA Mwenye Nguvu Zote.
[12] [l]“Lakini mnalinajisi Jina langu kwa
kusema kuhusu meza ya Bwana, ‘Imetiwa
unajisi pamoja na chakula chake. Ni ya
kudharauliwa.’ [13] [m]Nanyi mnasema, ‘Mzigo
gani huu!’ Nanyi mnaidharau kwa kiburi,”
asema BWANA Mwenye Nguvu Zote.
“Wakati mnapowaleta wanyama
mliopokonya kwa nguvu, walio vilema au
walio wagonjwa na kuwatoa kama dhabihu,

[a]**1:1** Nah 1:1; Mdo 7:38; Rum 3:1-2; 1Pet 4:11
[b]**1:2** Kum 4:37; Mal 2:14-17; 3:7-13; Yer 46:27; Rum 9:13; Mwa 25:23; 28:13
[c]**1:3** Lk 14:26; Eze 35:3; Isa 34:10; 13:22
[d]**1:4** Isa 11:14; 34:11; 9:10; 34:5; Mao 4:22; Eze 25:12-14; 26; 14
[e]**1:5** Za 35:17; 48:1; Mik 5:4; Isa 45:22; 52:10; Amo 1:11-12; Za 83:18
[f]**1:6** Law 20:9; Mt 15:14; 23:9; Lk 6:46; Ay 5:17; Kum 31; 12; 20:12; 5:16; Efe 6:2; Lk 18:20
[g]**1:7** Law 21:6; Eze 23; 41; 41:22
[h]**1:8** Law 1:3; Kum 15:21; Mwa 32:20; Isa 43:23; Ay 42:8
[i]**1:9** Law 23:33-44; Za 51:17; Mik 6:6-8; Rum 12; 1; Ebr 13:16; Yer 6:20; Hos 13:9
[j]**1:10** 2Nya 28:24; Hos 5:6; Mal 2:12; Law 22; 20; Isa 1:11-14; Yer 14:12; 1Kor 9:13; Flp 3:18-19
[k]**1:11** Isa 24:15; 56:6; 6:3; 12:4; 60:6-7; 19:21; Za 113:3; Mt 8:11; Ufu 5:8; Ebr 13:15; Isa 59:19; 66:19; Yn 4:21; 1Tim 2:8
[l]**1:12** Eze 41:22
[m]**1:13** Isa 43:22-24; Hes 14:11; Kum 15:21; Law 22:20; Isa 1:12

je, niwakubali kutoka mikononi mwenu?”
asema BWANA. 14 [a]“Amelaaniwa yeye
adanganyaye, aliye na mnyama wa kiume
anayekubalika katika kundi lake na kuweka
nadhiri ya kumtoa, lakini akatoa dhabihu
ya mnyama aliye na dosari kwa BWANA.
Kwa kuwa mimi ni Mfalme Mkuu, nalo Jina
langu linapaswa kuogopwa miongoni mwa
mataifa,” asema BWANA Mwenye Nguvu
Zote.

*Onyo Kwa Makuhani*

2 “Sasa onyo hili ni kwa ajili yenu, enyi
makuhani. 2 [b]Kama hamtasikiliza, na
kama hamtaki kuielekeza mioyo yenu
kuheshimu Jina langu, nitatuma laana
juu yenu, nami nitalaani baraka zenu.
Naam, nimekwisha kuzilaani, kwa sababu
hamkuielekeza mioyo yenu kuniheshimu
mimi,” Asema BWANA Mwenye Nguvu Zote.
3 “Kwa sababu yenu nitawakatilia mbali
wazao wenu. Nitazipaka nyuso zenu mavi,
mavi ya dhabihu zenu. Nanyi mtafukuzwa
pamoja nazo mtoke mbele zangu. 4 Nanyi
mtajua kuwa nimewapelekea onyo hili
ili kwamba Agano langu na Lawi lipate
kuendelea,” asema BWANA Mwenye
Nguvu Zote. 5 [c]“Agano langu lilikuwa
pamoja naye, agano la uhai na amani, nami
nilimpa yote, ili aniche na kuniheshimu,
naye akaniheshimu na kusimama akilicha
Jina langu. 6 [d]Fundisho la kweli lilikuwa
kinywani mwake, wala hakuna uongo
wowote uliopatikana katika midomo yake.
Alitembea nami katika amani na unyofu,
naye akawageuza wengi kutoka dhambini.
7 [e]“Kwa maana yapasa midomo ya
kuhani kuhifadhi maarifa. Tena kutoka
kinywani mwake watu wangepaswa
kutafuta mafundisho, kwa sababu yeye ni
mjumbe wa BWANA Mwenye Nguvu Zote.
8 [f]Lakini mmegeuka mkaiacha njia, na kwa
mafundisho yenu mmesababisha wengi
kujikwaa. Mmevunja agano na Lawi,”
asema BWANA Mwenye Nguvu Zote. 9 “Kwa
hiyo nimewasababisha ninyi kudharauliwa
na kufedheheshwa mbele ya watu wote,
kwa sababu hamkufuata njia zangu, bali
mmeonyesha upendeleo katika mambo ya
sheria.”

*Yuda Si Mwaminifu*

10 [g]Je, sote hatuna Baba mmoja?
Hatukuumbwa na Mungu mmoja? Kwa
nini basi tunalinajisi Agano la baba zetu
kwa kukosa uaminifu kila mmoja kwa
mwenzake?
11 [h]Yuda amevunja uaminifu. Jambo
la kuchukiza limetendeka katika Israeli
na katika Yerusalemu: Yuda amepanajisi
mahali patakatifu apendapo BWANA, kwa
kuoa binti wa mungu mgeni. 12 Kwa maana
kwa mtu yeyote atendaye jambo hili,
BWANA na amkatilie mbali kutoka hema
za Yakobo, hata kama huwa anamletea
BWANA Mwenye Nguvu Zote sadaka.
13 [i]Kitu kingine mnachokifanya:
Mnaifurikisha madhabahu ya BWANA kwa
machozi. Mnalia na kuugua kwa sababu
yeye haziangalii tena sadaka zenu wala
hazikubali kwa furaha kutoka mikononi
mwenu. 14 [j]Mnauliza, “Kwa nini?” Ni kwa
sababu BWANA ni shahidi kati yako na mke
wa ujana wako, kwa sababu umevunja
uaminifu naye, ingawa yeye ni mwenzako,
mke wa agano lako la ndoa.
15 [k]Je, BWANA hakuwafanya wao kuwa
mmoja? Katika mwili na katika roho wao
ni wa Mungu. Kwa nini wawe mmoja?
Kwa sababu Mungu alikuwa akitafuta
mzao mwenye kumcha Mungu. Kwa hiyo
jihadharini wenyewe katika roho zenu, mtu
asivunje uaminifu kwa mke wa ujana wake.

[a]**1:14** Kut 12:5; Za 95:3; 72:6-11; Oba 1:21; Law 22:18-21; Mdo 5:1
[b]**2:2** Kum 28:15
[c]**2:5** Hes 25:12; Kum 33:8
[d]**2:6** Dan 12:3; Lk 1:16-17; Yak 5:20
[e]**2:7** Kum 17:9; Isa 42:19; Hag 1:13; Gal 4:14
[f]**2:8** 1Sam 2:17
[g]**2:10** Isa 51:2; Mt 3:9; 1Kor 8:6; Ebr 12:9; Za 100:3
[h]**2:11** Neh 13:23
[i]**2:13** Yer 11:11; 14:12; Za 39:12; 66:18; Isa 58:2
[j]**2:14** Mwa 21:30; 24:22; Mit 5:18; Ebr 13:4
[k]**2:15** Mwa 2:24; Mt 19:4-6; Kum 14:2; 4:15; 1Kor 7:14; 7:10; Isa 54:6; Ebr 13:4

16 [a]“Ninachukia kuachana,” asema
BWANA, Mungu wa Israeli, “pia nachukia
mtu anayejivika jeuri kama vazi,” asema
BWANA Mwenye Nguvu Zote.

Kwa hiyo jihadharini wenyewe katika
roho zenu, wala msije mkavunja uaminifu.

*Siku Ya Hukumu*

17 [b]Mmemchosha BWANA kwa maneno
yenu.

Nanyi mnauliza, “Tumemchosha kwa
namna gani?”

Mmemchosha kwa kusema, “Wote
watendao mabaya ni wema machoni
pa BWANA, naye anapendezwa nao” au
“Mungu wa haki yuko wapi?”

3 [c]“Angalieni, nitamtuma mjumbe wangu,
atakayeiandaa njia mbele yangu. Ndipo
ghafula Bwana mnayemtafuta atakuja
hekaluni mwake. Mjumbe wa Agano,
ambaye mnamwonea shauku, atakuja,”
asema BWANA Mwenye Nguvu Zote.

2 [d]Lakini ni nani atakayeweza kustahimili
hiyo siku ya kuja kwake? Ni nani awezaye
kusimama atakapotokea? Kwa kuwa
atakuwa kama moto wa mfua fedha au kama
sabuni ya afuaye nguo. 3 [e]Ataketi kama
mfuaji na asafishaye fedha. Atawatakasa
Walawi, naye atawasafisha kama dhahabu
na fedha. Kisha BWANA atakuwa na watu
watakaoleta sadaka katika haki, 4 [f]nazo
sadaka za Yuda na Yerusalemu zitakubalika
kwa BWANA, kama katika siku zilizopita,
kama katika miaka ya zamani.

5 [g]“Basi nitakuja karibu nanyi ili
kuhukumu. Nami nitakuwa mwepesi
kushuhudia dhidi ya wachawi, wazinzi,
waapao kwa uongo, wanaopunja vibarua
malipo yao, wanaowaonea wajane na
yatima, na wanaowanyima wageni haki,
lakini hawaniogopi mimi,” asema BWANA
Mwenye Nguvu Zote.

*Kumwibia Mungu*

6 [h]“Mimi BWANA sibadiliki. Kwa
hiyo ninyi, enyi uzao wa Yakobo,
hamjaangamizwa. 7 [i]Tangu wakati wa
baba zenu mmegeukia mbali na amri zangu
nanyi hamkuzishika. Nirudieni mimi, nami
nitawarudia ninyi,” asema BWANA Mwenye
Nguvu Zote.

“Lakini mnauliza, ‘Tutarudi kwa namna
gani?’

8 [j]“Je, mwanadamu atamwibia Mungu?
Hata hivyo mnaniibia mimi.

“Lakini mnauliza, ‘Tunakuibia kwa
namna gani?’

“Mnaniibia zaka na dhabihu. 9 [k]Mko
chini ya laana, ninyi taifa lote, kwa
sababu mnaniibia mimi. 10 [l]Leteni zaka
kamili ghalani, ili kuwe na chakula katika
nyumba yangu. Nijaribuni katika hili,”
asema BWANA Mwenye Nguvu Zote, “nanyi
mwone kama sitawafungulia madirisha ya
mbinguni na kuwamwagieni baraka nyingi
mpaka mkose nafasi ya kutosha. 11 [m]Nami
kwa ajili yenu nitamkemea yeye alaye,
wala hataharibu mazao ya ardhi yenu, wala
mzabibu wenu hautapukutisha matunda

[a]**2:16** Kum 24:1; Mt 5:31-32; 19:4-9; Isa 58:4; Mk 10:4-5; Mwa 6:11; 34:25; Mit 4:17; Za 51:10
[b]**2:17** Isa 1:14; Eze 18:25; Za 5:4; Ay 8:3; Mwa 18:25
[c]**3:1** Hes 27:21; 2Nya 36:15; Isa 40:3; 63:9; Mt 11; 10; 3:3; Lk 7:27; Mik 5:2; 1Sam 9:20; Mdo 7:38; Hag 2:7
[d]**3:2** Eze 7:7; 22:14; Ufu 6:17; Dan 7:13; Yoe 2:31; Mt 16:27; Yak 5:8; 2Pet 3:4; 1Sam 6:20; Isa 1:31; 30:30; 4:4; Zek 13:9; Mt 3:10-12; Ay 9:30
[e]**3:3** Eze 12:10; 1Kor 3:13; 1Nya 23:28; Isa 1:25; Ay 28:1; Za 12:6; 132:9; Ufu 3:18; Zek 13:9; Rum 15:16; 1Pet 2:5
[f]**3:4** 2Nya 7:3; 7:12; Za 51:19; Eze 20:40; Mal 1:11
[g]**3:5** Kut 7:11; 20:14; Yak 2:11; 5:4-9; Isa 1:2; 47:9; 2Pet 2:12-14; Law 19:11-13; Yer 7:9; Yak 5:4; Kut 22:21-22; Kum 24:19; 31:12; Eze 22:7
[h]**3:6** Hes 23:19; Ebr 7:21; Yak 1:17; Ay 34:15; Hos 11:9; 1Sam 15:29; Rum 11:29; Mao 3:22
[i]**3:7** Kut 32:8; Mdo 7:51; Yer 7:26; Isa 44:22; Kum 30:1-4; Isa 55:6-7; Eze 18:32; Yak 4:8; Zek 1:3
[j]**3:8** Zek 5:3; Law 27:30; Hes 18:21; Neh 13:10-12; Lk 18:12
[k]**3:9** Kum 28:15-68; 11:26; Zek 5:3
[l]**3:10** Kut 22:29; Neh 13:12; 2Fal 7:2; Isa 44:3; Yoe 2:14, 24; 2Kor 9:8-11; Law 25:21; Mit 3:9; Mwa 7:11; 1Nya 26:29
[m]**3:11** Kut 10:15; 23:26; Kum 28:39; Amo 4:9

yake kabla ya wakati wake," asema Bwana
Mwenye Nguvu Zote. 12 [a]"Ndipo mataifa
yote yatawaita mliobarikiwa, kwa maana
nchi yenu itakuwa ya kupendeza sana,"
asema Bwana Mwenye Nguvu Zote.
13 [b]"Mmesema vitu vigumu dhidi yangu,"
asema Bwana.

"Hata hivyo mnauliza, 'Tumesema nini
dhidi yako?'
14 [c]"Mmesema, 'Ni bure kumtumikia
Mungu. Tumepata faida gani kwa
kushika maagizo yake na kwenda kama
waombolezaji mbele za Bwana Mwenye
Nguvu Zote? 15 [d]Lakini sasa wenye kiburi
wanabarikiwa. Hakika watenda mabaya
wanastawi, pia hata wale wanaoshindana
na Mungu ndio wanaosalimika.' "
16 [e]Ndipo wale waliomcha Bwana
wakasemezana wao kwa wao, naye
Bwana akasikiliza na akasikia. Kitabu
cha kumbukumbu kikaandikwa mbele yake
kuhusu wale ambao walimcha Bwana na
kuliheshimu jina lake.
17 [f]"Nao watakuwa watu wangu," asema
Bwana Mwenye Nguvu Zote, "katika siku
ile nitakapowafanya watu kuwa hazina
yangu. Nitawahurumia, kama vile kwa
huruma mtu amhurumiavyo mwanawe
anayemtumikia. 18 [g]Kwa mara nyingine
tena utaona tofauti kati ya wenye haki
na waovu, kati ya wale wanaomtumikia
Mungu na wale wasiomtumikia.

*Siku Ya Bwana*

4 [h]"Hakika siku inakuja, itawaka kama
tanuru. Wote wenye kiburi na kila
mtenda mabaya watakuwa mabua makavu,
na siku ile inayokuja itawawasha moto,"
asema Bwana Mwenye Nguvu Zote.
"Hakuna mzizi wala tawi litakalosalia
kwao. 2 [i]Bali kwenu ninyi mnaoliheshimu
Jina langu, jua la haki litawazukia, lenye
kuponya katika mabawa yake. Nanyi
mtatoka nje na kurukaruka kama ndama
aliyeachiwa kutoka zizini. 3 [j]Kisha ninyi
mtawakanyaga waovu, nao watakuwa
majivu chini ya nyayo za miguu yenu siku
ile nitakayofanya mambo haya," asema
Bwana Mwenye Nguvu Zote.
4 [k]"Kumbukeni sheria ya mtumishi wangu
Mose, amri na sheria nilizompa huko
Horebu kwa ajili ya Israeli wote.
5 [l]"Tazama, nitawapelekea nabii Eliya
kabla ya kuja siku ile iliyo kuu na ya kutisha
ya Bwana. 6 [m]Ataigeuza mioyo ya baba
iwaelekee watoto wao, na mioyo ya watoto
iwaelekee baba zao, la sivyo nitakuja na
kuipiga nchi kwa laana."

---

[a]**3:12** Kum 28:3-12; Isa 61:9; 62:4; Eze 20:6; Dan 8:9; 2Nya 31:10
[b]**3:13** Mal 2:17
[c]**3:14** Za 73:13; 100:2; Isa 1:14; 57:10; 58:3; Yn 12:26; Rum 12:11; Yos 22:5; Sef 1:12; Ay 21:14
[d]**3:15** Za 119:21; 14:1; 36:1-2; Yer 7:10; Ay 21:7
[e]**3:16** Za 34:15; 56:8; 87:6; 33:18; Kut 32:32; Lk 10:20; Mit 1:7; Ebr 3:13; Kum 31:12; Ufu 11:18; Mwa 22:12; 1Fal 18:3, 12
[f]**3:17** Isa 43:21; 26:20; Kut 8:22; Kum 7:6; Tit 2:14; Neh 13:22; Rum 8:14, 32; Za 103:13; Lk 15:1-32
[g]**3:18** Mwa 18:25; Kum 32:4; Mt 25:32-33

[h]**4:1** Isa 2:12; 5:24; 1:31; 2Fal 10:11; Nah 1:10; Eze 17:8; Mt 3:10
[i]**4:2** Kum 28:58; 2Pet 1:19; Za 61:5; 111:9; 118:27; 2Nya 7:14; Ufu 14:1; 22:2; Isa 9:2; 45:8; 30:26; Lk 1:78; Efe 5:14; Mt 4:23
[j]**4:3** Ay 40:12; Za 18:40-42; Eze 28:18; Mik 7:10
[k]**4:4** Kum 28:61; 4:10; Za 147:19; Mt 5:17; 7:12; Rum 2:13; 4:15
[l]**4:5** 1Fal 17:1; Yoe 2:31; Mt 11:14; 16:14
[m]**4:6** Dan 9:26; Lk 19:27, 43; 21:20; Mk 13:14; Lk 1:17; Zek 5:3; Isa 11:4; Ufu 19:15; Kum 13:15; Yos 6:17; 23:15; 4:2

# AGANO JIPYA

# MATHAYO

*Kumbukumbu Za Ukoo Wa Yesu Kristo*

**(Luka 3:23-38)**

1 [a]Habari za ukoo wa Yesu Kristo mwana wa Daudi, mwana wa Abrahamu:

2 [b]Abrahamu akamzaa Isaki,
Isaki akamzaa Yakobo,
Yakobo akawazaa Yuda na ndugu zake,
3 [c]Yuda akawazaa Peresi na Zera, ambao mama yao alikuwa Tamari,
Peresi akamzaa Hesroni,
Hesroni akamzaa Aramu,
4 Aramu akamzaa Aminadabu,
Aminadabu akamzaa Nashoni,
Nashoni akamzaa Salmoni,
5 [d]Salmoni akamzaa Boazi, na mama yake Boazi alikuwa Rahabu,
Boazi akamzaa Obedi, ambaye mama yake alikuwa Ruthu,
Obedi akamzaa Yese,
6 [e]Yese akamzaa Daudi ambaye alikuwa mfalme.

Daudi akamzaa Solomoni, ambaye mama yake ni yule aliyekuwa mke wa Uria.
7 [f]Solomoni akamzaa Rehoboamu,
Rehoboamu akamzaa Abiya,
Abiya akamzaa Asa,
8 Asa akamzaa Yehoshafati,
Yehoshafati akamzaa Yoramu,[g]
Yoramu akamzaa Uzia,
9 Uzia akamzaa Yothamu,
Yothamu akamzaa Ahazi,
Ahazi akamzaa Hezekia,
10 [h]Hezekia akamzaa Manase,
Manase akamzaa Amoni,
Amoni akamzaa Yosia,
11 [i]wakati wa uhamisho wa Babeli, Yosia alimzaa Yekonia na ndugu zake.

12 [j]Baada ya uhamisho wa Babeli:
Yekonia alimzaa Shealtieli,
Shealtieli akamzaa Zerubabeli,
13 Zerubabeli akamzaa Abiudi,
Abiudi akamzaa Eliakimu,
Eliakimu akamzaa Azori,
14 Azori akamzaa Sadoki,
Sadoki akamzaa Akimu,
Akimu akamzaa Eliudi,
15 Eliudi akamzaa Eleazari,
Eleazari akamzaa Matani,
Matani akamzaa Yakobo,
16 [k]naye Yakobo akamzaa Yosefu ambaye alikuwa mumewe Maria, mama yake Yesu, aitwaye Kristo.[l]

17 Hivyo, kulikuwepo na jumla ya vizazi kumi na vinne tangu Abrahamu mpaka Daudi, vizazi kumi na vinne tangu Daudi hadi wakati wa uhamisho kwenda utumwani Babeli, na vizazi kumi na vinne tangu wakati wa uhamisho kwenda utumwani Babeli hadi Kristo.

*Kuzaliwa Kwa Yesu Kristo*

**(Luka 2:1-7)**

18 [m]Basi Kuzaliwa kwake Yesu Kristo kulikuwa hivi: Maria mama yake alikuwa ameposwa na Yosefu, lakini kabla hawajakutana kimwili, Maria alionekana kuwa na mimba kwa uweza wa Roho
Mtakatifu. 19 [n]Kwa kuwa Yosefu, mwanaume aliyekuwa amemposa alikuwa mtu

[a]**1:1** Rum 1:3; Mwa 22:18; Lk 3:23-38
[b]**1:2** Mwa 21:3, 12; 25:26; 29:35; 49:10
[c]**1:3** Mwa 38:27-30; 1Nya 2:5, 9; Rut 4:18-22; 1Nya 2:10-12
[d]**1:5** Rut 4:13-17; Ebr 11:31
[e]**1:6** 1Sam 16:1; 17:12; 2Sam 12:24
[f]**1:7** 1Nya 3:10-14
[g]8 *Yoramu* ndiye *Yehoramu,* maana yake ni *Yehova yu juu.*
[h]**1:10** 2Fal 20:21; 1Nya 3:13
[i]**1:11** Dan 1:1-2; 2Fal 24:14-16; Yer 27:20; 40:1
[j]**1:12** 1Nya 3:17-19; Ezr 3:2
[k]**1:16** Lk 1:27; Mt 27:17
[l]16 *Kristo* maana yake ni *Masiya,* yaani *Aliyetiwa mafuta.*
[m]**1:18** Lk 1:35
[n]**1:19** Kum 24:1

mwadilifu, hakutaka kumwaibisha Maria
hadharani, aliazimu kumwacha kwa siri.
20 [a]Lakini mara alipoazimu kufanya
jambo hili, malaika wa Bwana akamtokea
katika ndoto na kusema, "Yosefu mwana
wa Daudi, usiogope kumchukua Maria
awe mke wako, kwa maana mimba aliyo
nayo ni kwa uweza wa Roho Mtakatifu.
21 [b]Naye atamzaa mwana, nawe utamwita
Jina lake Yesu,[c] kwa maana yeye ndiye
atakayewaokoa watu wake kutoka dhambi
zao."
22 [d]Haya yote yalitukia ili litimie lile
Bwana alilokuwa amenena kupitia nabii,
akisema: 23 [e]"Tazama, bikira atachukua
mimba, naye atamzaa mwana, nao
watamwita Jina lake Imanueli": maana
yake, "Mungu pamoja nasi."
24 [f]Yosefu alipoamka kutoka usingizini,
akafanya kama vile alivyoagizwa na malaika
wa Bwana, akamchukua Maria kuwa mke
wake. 25 [g]Lakini hawakukutana kimwili
mpaka Maria alipojifungua mwanawe
kifungua mimba akamwita Jina lake Yesu.

### *Wataalamu Wa Nyota Wafika Kumwona Mtoto Yesu*

2 [h]Baada ya Yesu kuzaliwa katika mji wa
Bethlehemu huko Uyahudi, wakati wa
utawala wa Mfalme Herode, wataalamu wa
mambo ya nyota kutoka mashariki walifika
Yerusalemu 2 [i]wakiuliza, "Yuko wapi
huyo aliyezaliwa mfalme wa Wayahudi?
Kwa maana tumeona nyota yake ikitokea
mashariki, nasi tumekuja kumwabudu."
3 Mfalme Herode aliposikia jambo hili
aliingiwa na hofu sana pamoja na watu wote
wa Yerusalemu. 4 [j]Herode akawaita pamoja
viongozi wa makuhani na walimu wa sheria,
akawauliza ni mahali gani ambapo Kristo[k]
angezaliwa. 5 [l]Nao wakamwambia, "Katika
Bethlehemu ya Uyahudi, kwa maana hivyo
ndivyo ilivyoandikwa na nabii:

6 [m]" 'Nawe, Bethlehemu, katika nchi ya
Yuda,
wewe si mdogo miongoni
mwa watawala wa Yuda;
kwa maana kutoka kwako atakuja
mtawala
atakayekuwa mchungaji
wa watu wangu Israeli.' "

7 Ndipo Herode akawaita wale wataalamu
wa nyota kwa siri na kutaka kujua kutoka
kwao uhakika kamili wa wakati ile nyota
ilionekana. 8 Kisha akawatuma waende
Bethlehemu akiwaambia, "Nendeni
mkamtafute kwa bidii huyo mtoto. Nanyi
mara mtakapomwona, mniletee habari ili
na mimi niweze kwenda kumwabudu."
9 Baada ya kumsikia mfalme, wale
wataalamu wa nyota wakaenda zao, nayo ile
nyota waliyoiona mashariki ikawatangulia,
nao wakaifuata mpaka iliposimama mahali
pale alipokuwa mtoto. 10 Walipoiona ile
nyota wakajawa na furaha kubwa mno.
11 [n]Walipoingia ndani ya ile nyumba,
wakamwona mtoto pamoja na Maria mama
yake, wakamsujudu na kumwabudu yule
mtoto Yesu. Ndipo wakafungua hazina zao,
wakamtolea zawadi za dhahabu, uvumba
na manemane. 12 [o]Nao wakiisha kuonywa
katika ndoto wasirudi kwa Herode,
wakarudi kwenda katika nchi yao kwa njia
nyingine.

### *Yosefu, Maria Na Mtoto Yesu Wakimbilia Misri*

13 [p]Walipokwisha kwenda zao, malaika
wa Bwana akamtokea Yosefu katika ndoto
akamwambia, "Ondoka, mchukue mtoto na
mama yake mkimbilie Misri. Kaeni huko

[a]**1:20** Lk 1:35
[b]**1:21** Lk 1:31; Za 130:8; Tit 2:14
[c]21 *Yesu* ni *Iesous* kwa Kiyunani, na kwa Kiebrania ni *Yoshua* au *Yeshua.* Maana yake ni *Yehova ni wokovu.*
[d]**1:22** Mt 22:15; 17:23; 4:14; Lk 4:21; 21:22; Yn 13:18; 19:24
[e]**1:23** Isa 7:14; 8:8-10
[f]**1:24** Mdo 5:19
[g]**1:25** Lk 1:31; 2:7; 2:1; 2:4-7; 1:5
[h]**2:1** Lk 2:4, 6; Mwa 10:30; 25:6; 1Fal 4:30
[i]**2:2** Yer 23:5; Yn 1:49; Hes 24:17
[j]**2:4** 2Nya 36:14; 34:13; Mal 2:7
[k]4 *Kristo* maana yake ni *Masiya,* yaani *Aliyetiwa mafuta.*
[l]**2:5** Yn 7:42; Mik 5:2
[m]**2:6** Mik 5:2; 2Sam 5:2; Yn 7:42; Ufu 2:27
[n]**2:11** Isa 60:3; Za 72:10
[o]**2:12** Ebr 11:7; Mt 2:13; 2:19; 2:22; 27:19
[p]**2:13** Mdo 5:19; Mt 27:19

mpaka nitakapowaambia, kwa maana
Herode anataka kumtafuta huyu mtoto ili
amuue."
14 Kisha Yosefu akaondoka, akamchukua
mtoto pamoja na mama yake wakati wa
usiku, nao wakaenda Misri 15 [a]ambako
walikaa mpaka Herode alipofariki. Hili
lilifanyika ili litimie lile lililonenwa na
Bwana kwa kinywa cha nabii kusema:
"Nilimwita mwanangu kutoka Misri."
16 Herode alipong'amua kwamba wale
wataalamu wa nyota wamemshinda kwa
akili, alikasirika sana, naye akatoa amri ya
kuwaua watoto wote wa kiume wenye umri
wa miaka miwili kurudi chini katika mji
wa Bethlehemu na sehemu zote za jirani,
kufuatana na ule muda alioambiwa na wale
wataalamu wa nyota. 17 [b]Ndipo lilipotimia
neno lililonenwa na nabii Yeremia.

18 [c]"Sauti ilisikika huko Rama,
maombolezo na kilio kikubwa,
Raheli akilia kwa ajili ya wanawe,
akikataa kufarijiwa,
kwa sababu hawako tena."

*Kurudi Kutoka Misri*

19 [d]Baada ya Herode kufa, malaika wa
Bwana akamtokea Yosefu katika ndoto huko
Misri 20 na kusema, "Ondoka, mchukue
mtoto na mama yake mwende, mrudi katika
nchi ya Israeli kwa sababu wale waliokuwa
wanatafuta uhai wa mtoto wamekufa."
21 Basi Yosefu, akaondoka akamchukua
mtoto na mama yake wakaenda mpaka
nchi ya Israeli. 22 [e]Lakini aliposikia kwamba
Arkelao alikuwa anatawala huko Uyahudi
mahali pa Herode baba yake, aliogopa
kwenda huko. Naye akiisha kuonywa
katika ndoto, akaenda zake sehemu za
Galilaya, 23 [f]akaenda akaishi katika mji
ulioitwa Nazareti. Hivyo likawa limetimia
neno lililonenwa na manabii, "Ataitwa
Mnazarayo."

[a]**2:15** Hes 11:1; Kut 4:22-23
[b]**2:17** Yer 31:15; Mt 2:17, 23; 1:2
[c]**2:18** Mwa 35:19
[d]**2:19** Mt 27:19
[e]**2:22** Mt 27:19; Lk 2:39
[f]**2:23** Lk 1:26; Isa 11:1; Yn 1:46

*Yohana Mbatizaji Atayarisha Njia*

**(Marko 1:1-8; Luka 3:1-18; Yohana 1:19-28)**

3 [g]Siku hizo Yohana Mbatizaji alikuja
akihubiri katika nyika ya Uyahudi,
akisema, 2 [h]"Tubuni, kwa maana Ufalme
wa Mbinguni umekaribia." 3 [i]Huyu ndiye
yule aliyenenwa habari zake na nabii Isaya
aliposema:

"Sauti ya mtu aliaye huko nyikani,
'Tayarisheni njia kwa ajili ya Bwana,
yanyoosheni mapito yake.' "

4 [j]Basi Yohana alivaa mavazi
yaliyotengenezwa kwa singa za ngamia,
akiwa na mkanda wa ngozi kiunoni mwake.
Chakula chake kilikuwa nzige na asali ya
mwitu. 5 [k]Watu walikuwa wakimwendea
kutoka Yerusalemu, Uyahudi yote na nchi
zote za kandokando ya Mto Yordani. 6 [l]Nao
wakaziungama dhambi zao, akawabatiza
katika Mto Yordani.
7 [m]Lakini alipowaona Mafarisayo na
Masadukayo wengi wakija ili kubatizwa,
aliwaambia: "Ninyi watoto wa nyoka! Ni
nani aliyewaonya kuikimbia ghadhabu
inayokuja? 8 [n]Basi zaeni matunda
yastahiliyo toba. 9 [o]Wala msidhani mnaweza
kusema mioyoni mwenu kuwa, 'Sisi tunaye
Abrahamu, baba yetu.' Nawaambia kuwa
Mungu anaweza kumwinulia Abrahamu
watoto kutoka kwa mawe haya. 10 [p]Hata
sasa shoka limeshawekwa tayari kwenye
shina la kila mti, basi kila mti usiozaa
matunda mazuri, hukatwa na kutupwa
motoni.
11 [q]"Mimi nawabatiza kwa maji kwa
ajili ya toba. Lakini nyuma yangu anakuja
yeye aliye na uwezo kuliko mimi, ambaye
sistahili hata kuvichukua viatu vyake. Yeye

[g]**3:1** Lk 3:2-19
[h]**3:2** Dan 7:14; Lk 17:20
[i]**3:3** Mal 3:1; Yn 1:23
[j]**3:4** 1Fal 1:8
[k]**3:5** Mk 1:5; Lk 3:7
[l]**3:6** Mdo 19:4, 18; Mk 1:4
[m]**3:7** Mt 12:34; 23:33; Rum 1:18; 1The 1:10
[n]**3:8** Mdo 26:20
[o]**3:9** Rum 2:28-29
[p]**3:10** Lk 3:9; Yn 15:2-6
[q]**3:11** Mk 1:18; Isa 4:4; Mdo 2:3-4

atawabatiza kwa Roho Mtakatifu[a] na kwa
moto. 12 [b]Pepeto lake liko mkononi mwake,
naye atasafisha sakafu yake ya kupuria, na
kuikusanya ngano ghalani na kuyateketeza
makapi kwa moto usiozimika.”

*Yesu Abatizwa*

**(Marko 1:9-11; Luka 3:21-22)**

13 [c]Kisha Yesu akaja kutoka Galilaya
mpaka Mto Yordani ili Yohana ambatize.
14 Lakini Yohana akajitahidi kumzuia,
akimwambia, “Mimi ninahitaji kubatizwa
na wewe, nawe waja kwangu nikubatize?”
15 Lakini Yesu akamjibu, “Kubali hivi
sasa, kwa maana ndivyo itupasavyo kwa
njia hii kuitimiza haki yote.” Hivyo Yohana
akakubali.
16 [d]Naye Yesu alipokwisha kubatizwa,
mara alipotoka ndani ya maji, ghafula
mbingu zikafunguka, akamwona Roho
wa Mungu akishuka kama hua na kutulia
juu yake. 17 [e]Nayo sauti kutoka mbinguni
ikasema, “Huyu ni Mwanangu mpendwa,
ambaye ninapendezwa sana naye.”

*Kujaribiwa Kwa Yesu*

**(Marko 1:12-13; Luka 4:1-13)**

4 [f]Kisha Yesu akaongozwa na Roho
Mtakatifu kwenda nyikani ili akajaribiwe
na ibilisi. 2 [g]Baada ya kufunga siku arobaini
usiku na mchana, hatimaye akaona njaa.
3 [h]Mjaribu akamjia na kumwambia, “Ikiwa
wewe ndiye Mwana wa Mungu, amuru
mawe haya yawe mikate.”
4 [i]Lakini Yesu akajibu, “Imeandikwa:
‘Mtu haishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno
litokalo katika kinywa cha Mungu.’ ”

5 [j]Ndipo ibilisi akamchukua Yesu mpaka
mji mtakatifu na kumweka juu ya mnara
mrefu wa Hekalu, 6 [k]akamwambia, “Kama
wewe ndiwe Mwana wa Mungu jitupe chini.
Kwa kuwa imeandikwa:

“ ‘Atakuagizia malaika zake,
nao watakuchukua mikononi
mwao
ili usije ukajikwaa mguu wako katika
jiwe.’ ”

7 [l]Yesu akamjibu, “Pia imeandikwa:
‘Usimjaribu Bwana Mungu wako.’ ”
8 Kwa mara nyingine, ibilisi akamchukua
Yesu mpaka kwenye kilele cha mlima
mrefu na kumwonyesha falme zote za
dunia na fahari zake, 9 kisha akamwambia,
“Nitakupa hivi vyote kama ukinisujudia na
kuniabudu.”
10 [m]Yesu akamwambia, “Ondoka mbele
yangu, Shetani! Kwa maana imeandikwa,
‘Mwabudu Bwana Mungu wako, na
umtumikie yeye peke yake.’ ”
11 [n]Ndipo ibilisi akamwacha, nao malaika
wakaja na kumhudumia.

*Yesu Aanza Kuhubiri*

**(Marko 1:14-15; Luka 4:14-15)**

12 [o]Yesu aliposikia kwamba Yohana
Mbatizaji alikuwa ametiwa gerezani, alirudi
Galilaya. 13 [p]Akaondoka Nazareti akaenda
kuishi Kapernaumu, mji ulioko karibu na
bahari, katika mipaka ya nchi ya Zabuloni
na Naftali, 14 [q]ili kutimiza unabii wa nabii
Isaya, kama alivyosema:

15 [r]“Nchi ya Zabuloni na nchi ya
Naftali,
kwenye njia ya kuelekea baharini,
ng’ambo ya Yordani,
Galilaya ya watu wa Mataifa:

---

[a]11 …*kwa Roho Mtakatifu* hapa ina maana ya *katika Roho Mtakatifu.*
[b]**3:12** Mt 13:30; 25:41
[c]**3:13** Mt 3:1; Mk 1:4; Yn 1:31-34
[d]**3:16** Isa 11:2; 42:1; Mk 1:10; Lk 3:22; Yn 1:32-33
[e]**3:17** Kum 4:12; Yn 12:28; Za 2:7; 2:7; Mdo 13:33; Isa 42:1; 2Pet 1:17
[f]**4:1** Kut 34:28; 1Fal 19:8
[g]**4:2** Kut 34:28; 1Fal 19:8
[h]**4:3** 1The 3:5; Mk 3:11; Ufu 2:18
[i]**4:4** Kum 8:3; Yn 4:34
[j]**4:5** Neh 11:1; Mt 27:5
[k]**4:6** Za 91:11-12; Mt 4:3
[l]**4:7** Kum 6:16
[m]**4:10** Ay 1:6-9; Rum 16:20; 6:13
[n]**4:11** Lk 22:43; Ebr 1:14
[o]**4:12** Mt 14:3; Mk 1:14
[p]**4:13** Mk 9:33; Yn 2:12
[q]**4:14** Isa 9:1, 2; 9:1; Mt 1:22
[r]**4:15** Isa 9:1, 2

16 [a]watu wale waliokaa gizani
wameona nuru kuu;
nao wale walioishi katika nchi ya
uvuli wa mauti,
nuru imewazukia.”

17 [b]Tangu wakati huo, Yesu alianza kuhubiri akisema: “Tubuni, kwa maana Ufalme wa Mbinguni umekaribia.”

*Yesu Awaita Wanafunzi Wake Wa Kwanza*

**(Marko 1:16-20; Luka 5:1-11)**

18 [c]Yesu alipokuwa anatembea kando
ya Bahari ya Galilaya, aliwaona ndugu
wawili, Simoni aitwaye Petro, na Andrea
ndugu yake. Walikuwa wakizitupa nyavu
zao baharini kwa kuwa wao walikuwa
wavuvi. 19 [d]Yesu akawaambia, “Njooni,
nifuateni nami nitawafanya mwe wavuvi
wa watu.” 20 [e]Mara wakaziacha nyavu zao,
wakamfuata.

21 [f]Alipoendelea mbele kutoka pale,
akawaona ndugu wengine wawili, Yakobo
mwana wa Zebedayo na Yohana nduguye,
wakiwa wamekaa kwenye mashua pamoja
na baba yao Zebedayo, wakizitengeneza
nyavu zao. Yesu akawaita. 22 [g]Nao mara
wakaiacha mashua yao, pamoja na baba
yao, wakamfuata.

*Yesu Ahubiri Na Kuponya Wagonjwa*

**(Luka 6:17-19)**

23 [h]Yesu akapita katika Galilaya yote,
akifundisha katika masinagogi yao,
akihubiri habari njema za Ufalme, na
akiponya kila ugonjwa na kila aina ya
maradhi miongoni mwa watu. 24 [i]Kwa hiyo
sifa zake zikaenea sehemu zote za Shamu,
nao watu wakamletea wote waliokuwa
na magonjwa mbalimbali na maumivu,
waliopagawa na pepo wachafu, wenye
kifafa na waliopooza, naye akawaponya.
25 [j]Makutano makubwa ya watu yakawa
yanamjia kutoka Galilaya, Dekapoli,[k]
Yerusalemu, Uyahudi na kutoka ng’ambo
ya Mto Yordani.

**MAHUBIRI YA YESU KWENYE MLIMA**

*(Mathayo 5–7)*

*Sifa Za Aliyebarikiwa*

**(Luka 6:20-23)**

1 [l]Basi Yesu alipoona makutano, alipanda
mlimani akaketi chini, nao wanafunzi wake
wakamjia. 2 Ndipo akaanza kuwafundisha,
akisema:

3 [m]“Heri walio maskini wa roho,
maana Ufalme wa Mbinguni ni
wao.
4 [n]Heri wale wanaohuzunika,
maana hao watafarijiwa.
5 [o]Heri walio wapole,
maana hao watairithi nchi.
6 [p]Heri wenye njaa na kiu ya haki,
maana hao watatoshelezwa.
7 [q]Heri wenye huruma,
maana hao watapata rehema.
8 [r]Heri walio na moyo safi,
maana hao watamwona Mungu.
9 [s]Heri walio wapatanishi,
maana hao wataitwa wana wa
Mungu.
10 [t]Heri wanaoteswa kwa sababu ya
haki,
maana Ufalme wa Mbinguni ni
wao.

11 [u]“Heri ninyi watu watakapowashutumu,
na kuwatesa na kunena dhidi yenu mabaya

[a]**4:16** Isa 9:1-2; Yn 1:4-9
[b]**4:17** Mt 3:2; Mk 1:14, 15
[c]**4:18** Mk 7:31; Yn 6:1; Mt 16:17-18
[d]**4:19** Lk 5:28; Yn 1:43
[e]**4:20** Mk 10:28; Lk 18:28; Mt 19:27
[f]**4:21** Mk 3:17; Lk 8:51
[g]**4:22** Mt 4:19
[h]**4:23** Mk 1:39; Lk 4:15, 44; 7:22; Yn 18:20; 3:10; Mk 1:14; Mdo 20; 25; 28:23, 31
[i]**4:24** Lk 2:2; Mk 1:32; 5:15-18; Mt 17:15; Mk 2:3
[j]**4:25** Mk 3:7-8; Lk 6:17
[k]25 Yaani Miji Kumi.
[l]**5:1** Mk 3:13, 20; Lk 6:20-49
[m]**5:3** Mt 5:10, 19; 25:34; Isa 57:15
[n]**5:4** Isa 61:2-3; Ufu 7:17
[o]**5:5** Za 37:11; Rum 4:13
[p]**5:6** Isa 55:1-2
[q]**5:7** Yak 2:13; Za 41:1; Mt 6:14; Mk 11:24
[r]**5:8** Za 24:3-4; 73:1; 17:15; Ebr 12:14
[s]**5:9** Mt 5:44, 45; Rum 8:14
[t]**5:10** 1Pet 3:14
[u]**5:11** Isa 51:7; 1Pet 4:14

ya aina zote kwa uongo kwa ajili yangu.
12 [a]Furahini na kushangilia kwa maana
thawabu yenu ni kubwa mbinguni, kwa
kuwa hivyo ndivyo walivyowatesa manabii
waliokuwa kabla yenu.

### *Chumvi Na Nuru*

**(Marko 9:50; Luka 14:34-35)**

13 [b]“Ninyi ni chumvi ya ulimwengu.
Lakini chumvi ikipoteza ladha yake,
yawezaje kurudishiwa ladha yake tena?
Haifai tena kwa kitu chochote, ila kutupwa
nje ikanyagwe na watu.
14 [c]“Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji
uliojengwa kilimani hauwezi kufichika.
15 [d]Wala watu hawawashi taa na kuifunika
kwa bakuli. Badala yake, huiweka kwenye
kinara chake, nayo hutoa mwanga kwa kila
mtu aliyemo ndani ya ile nyumba. 16 [e]Vivyo
hivyo, nuru yenu iangaze mbele ya watu,
ili wapate kuona matendo yenu mema
wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni.

### *Kutimiza Sheria*

17 [f]“Msidhani kwamba nimekuja kufuta
Sheria au Manabii; sikuja kuondoa bali
kutimiza. 18 [g]Kwa maana, amin nawaambia,
mpaka mbingu na dunia zitakapopita,
hakuna hata herufi moja ndogo wala
nukta itakayopotea kwa namna yoyote
kutoka kwenye Sheria, mpaka kila kitu
kiwe kimetimia. 19 [h]Kwa hiyo, yeyote
atakayevunja mojawapo ya amri ndogo
kuliko zote ya amri hizi, naye akawafundisha
wengine kufanya hivyo, ataitwa mdogo
kabisa katika Ufalme wa Mbinguni, lakini
yeyote azitendaye na kuzifundisha hizi amri
ataitwa mkuu katika Ufalme wa Mbinguni.
20 [i]Kwa maana nawaambia, haki yenu
isipozidi haki ya Mafarisayo na walimu wa
sheria, kamwe hamtaingia katika Ufalme
wa Mbinguni.

### *Kuhusu Hasira*

**(Luka 12:57-59)**

21 [j]“Mmesikia walivyoambiwa watu
wa zamani kwamba, ‘Usiue. Yeyote
atakayeua atapaswa hukumu.’ 22 [k]Lakini
mimi nawaambia kwamba, yeyote
atakayemkasirikia ndugu yake, atapaswa
hukumu. Tena, yeyote atakayemwambia
ndugu yake, ‘Raka,’[l] atapaswa kujibu
kwa Baraza la Wayahudi.[m] Lakini yeyote
atakayesema ‘Wewe mpumbavu!’ atapaswa
hukumu ya moto wa jehanamu.
23 [n]“Kwa hiyo, kama unatoa sadaka yako
madhabahuni, ukakumbuka kuwa ndugu
yako ana kitu dhidi yako, 24 [o]iache sadaka
yako hapo mbele ya madhabahu. Enda
kwanza ukapatane na ndugu yako; kisha
urudi na ukatoe sadaka yako.
25 [p]“Patana na mshtaki wako upesi
wakati uwapo njiani pamoja naye
kwenda mahakamani, ili mshtaki wako
asije akakutia mikononi mwa hakimu,
naye hakimu akakutia mikononi mwa
askari, nawe ukatupwa gerezani. 26 Amin,
nakuambia, hautatoka humo hadi uwe
umelipa senti ya mwisho.

### *Kuhusu Uzinzi*

27 [q]“Mmesikia kwamba ilinenwa, ‘Usizini.’
28 [r]Lakini mimi nawaambia kwamba, yeyote
amtazamaye mwanamke kwa kumtamani,
amekwisha kuzini naye moyoni mwake.
29 [s]Jicho lako la kuume likikusababisha

---

[a]**5:12** Za 9:2; 2Nya 36:16; 2Kor 6:10
[b]**5:13** Mk 9:50; Lk 14:34-35
[c]**5:14** Yn 8:12
[d]**5:15** Mk 4:21; Lk 11:33
[e]**5:16** Efe 5:8-9; 1Pet 2:12
[f]**5:17** Rum 3:31; 10:4; Gal 1:24
[g]**5:18** Za 119:89; Mk 13:31
[h]**5:19** Yak 2:10; 1Kor 15:9
[i]**5:20** Rum 9:31; 10:3
[j]**5:21** Kut 21:12; 5:17; Law 24:17
[k]**5:22** 1Yn 3:22; Yn 11:47; Mdo 6:12; Lk 16:24; Yak 3:6
[l]22 Raka ni neno la Kiaramu ambalo maana yake ni dharau au dhihaka ya hali ya juu.
[m]22 *Baraza la Wayahudi* lilikuwa kundi kuu kabisa la utawala wa Wayahudi lililoundwa na wazee 70 pamoja na kuhani mkuu.
[n]**5:23** Mt 8:4; 23:19; Mk 11:25
[o]**5:24** Ay 42:8; 18:19; 1Tim 2:8; 1Pet 3:7
[p]**5:25** Mt 18:35; Lk 12:58-59
[q]**5:27** Kut 20:14; Kum 5:18
[r]**5:28** Mit 6:25; 2Pet 2:14
[s]**5:29** Rum 14:21; 1Kor 8:13

kutenda dhambi, ling'oe ulitupe mbali. Ni
afadhali kwako kupoteza kiungo kimoja
cha mwili wako kuliko mwili wako mzima
ukatupwa jehanamu. 30 [a]Kama mkono
wako wa kuume ukikusababisha kutenda
dhambi, ukate, uutupe mbali. Ni afadhali
kwako kupoteza kiungo kimoja cha mwili
wako kuliko mwili wako mzima utupwe
jehanamu.

*Kuhusu Talaka*

**(Mathayo 19:9; Marko 10:11-12; Luka 16:18)**

31 [b]"Pia ilinenwa kwamba, 'Mtu yeyote
amwachaye mkewe sharti ampe hati ya
talaka.' 32 [c]Lakini mimi nawaambia, yeyote
amwachaye mkewe isipokuwa kwa kosa la
uasherati, amfanya mkewe kuwa mzinzi.
Na yeyote amwoaye yule mwanamke
aliyeachwa, anazini.

*Kuhusu Kuapa*

33 [d]"Tena mmesikia walivyoambiwa watu
wa zamani kwamba, 'Usiape kwa uongo, bali
timiza kiapo kile ulichofanya kwa Bwana.'
34 [e]Lakini mimi nawaambia, msiape kabisa:
iwe kwa mbingu, kwa kuwa ni kiti cha enzi
cha Mungu; 35 [f]au kwa dunia, kwa kuwa
ndipo mahali pake pa kuwekea miguu; au
kwa Yerusalemu, kwa kuwa ndio mji wa
Mfalme Mkuu. 36 Nanyi msiape kwa vichwa
vyenu, kwa kuwa hamwezi kuufanya hata
unywele mmoja kuwa mweupe au mweusi.
37 [g]'Ndiyo' yenu iwe 'Ndiyo,' na 'Hapana'
yenu iwe 'Hapana.' Lolote zaidi ya hili
latoka kwa yule mwovu.

*Kuhusu Kulipiza Kisasi*

**(Luka 6:29-30)**

38 [h]"Mmesikia kwamba ilinenwa, 'Jicho
kwa jicho na jino kwa jino.' 39 [i]Lakini mimi
nawaambia, msishindane na mtu mwovu.
Lakini kama mtu akikupiga kwenye shavu
la kuume, mgeuzie na la pili pia. 40 [j]Kama
mtu akitaka kukushtaki na kuchukua
joho lako, mwachie achukue na koti pia.
41 [k]Kama mtu akikulazimisha kwenda maili
moja, nenda naye maili mbili. 42 [l]Mpe yeye
akuombaye, wala usimgeuzie kisogo yeye
atakaye kukukopa.

*Upendo Kwa Adui*

**(Luka 6:27-28, 32-36)**

43 [m]"Mmesikia kwamba ilinenwa, 'Mpende
jirani yako na umchukie adui yako.'
44 [n]Lakini ninawaambia: Wapendeni adui
zenu na waombeeni wanaowatesa ninyi,
45 [o]ili mpate kuwa watoto wa Baba yenu aliye
mbinguni. Kwa maana yeye huwaangazia
jua lake watu waovu na watu wema,
naye huwanyeshea mvua wenye haki na
wasio haki. 46 [p]Kama mkiwapenda tu wale
wanaowapenda, mtapata thawabu gani?
Je, hata watoza ushuru hawafanyi hivyo?
47 Nanyi kama mkiwasalimu ndugu zenu tu,
je, mnafanya nini zaidi ya wengine? Je, hata
watu wasiomjua Mungu, hawafanyi hivyo?
48 [q]Kwa hiyo kuweni wakamilifu kama Baba
yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu.

*Kuwapa Wahitaji*

6 [r]"Angalieni msitende wema wenu mbele
ya watu ili wawaone. Kwa maana
mkifanya hivyo, hamna thawabu kutoka
kwa Baba yenu aliye mbinguni.
2 "Hivyo mnapowapa wahitaji, msipige
panda mbele yenu kama wafanyavyo
wanafiki katika masinagogi na mitaani,
ili wasifiwe na watu. Amin nawaambia
wao wamekwisha kupokea thawabu yao.

[a]**5:30** Mt 5:29
[b]**5:31** Kum 24:1-4
[c]**5:32** Lk 16:18
[d]**5:33** Law 19:12; Hes 30:2; Mt 23:16-22
[e]**5:34** Yak 5:12; Isa 66:1; Mt 23:22
[f]**5:35** Za 48:2
[g]**5:37** Yak 5:12; Efe 6:16; 1Yn 3:12
[h]**5:38** Law 24:20; Kum 19:21
[i]**5:39** 1Kor 6:7; 1Pet 3:9
[j]**5:40** 1Kor 6:7
[k]**5:41** Mt 27:32; Mk 15:21
[l]**5:42** Kum 15:8; Lk 16:30
[m]**5:43** Law 19:18; Gal 5:14; Kum 23:6; Za 139:21-22
[n]**5:44** Yn 15:20; Rum 8:35
[o]**5:45** Lk 6:35; Rum 8:14; Ay 25:3
[p]**5:46** Lk 6:32
[q]**5:48** Law 19:2; 1Pet 1:16
[r]**6:1** Mt 5:16; 23:5; Rum 12:8

3 [a]Lakini ninyi mtoapo sadaka, fanyeni kwa
siri, hata mkono wako wa kushoto usijue
mkono wako wa kuume unachofanya, 4 [b]ili
sadaka yako iwe ni siri. Ndipo Baba yako
wa mbinguni, yeye aonaye sirini atakupa
thawabu kwa wazi.

*Kuhusu Maombi*

**(Luka 11:2-4)**

5 [c]"Nanyi msalipo, msiwe kama wanafiki,
maana wao hupenda kusali wakiwa
wamesimama katika masinagogi na kando
ya barabara ili waonekane na watu. Amin
nawaambia, wao wamekwisha kupata
thawabu yao. 6 [d]Lakini wewe unaposali,
ingia chumbani mwako, funga mlango na
umwombe Baba yako aliye sirini. Naye Baba
yako aonaye sirini atakupa thawabu yako.
7 [e]Nanyi mnaposali msiseme maneno kama
wafanyavyo watu wasiomjua Mungu. Kwa
maana wao hudhani kwamba watasikiwa
kwa sababu ya wingi wa maneno yao.
8 [f]Msiwe kama wao, kwa sababu Baba
yenu anajua kile mnachohitaji kabla
hamjamwomba.
9 [g]"Hivi basi, ndivyo iwapasavyo kuomba:

" 'Baba yetu uliye mbinguni,
Jina lako litukuzwe.
10 Ufalme wako uje.
Mapenzi yako yafanyike
hapa duniani kama huko
mbinguni.
11 [h]Utupatie riziki yetu
ya kila siku.
12 [i]Utusamehe deni zetu,
kama sisi nasi tulivyokwisha
kuwasamehe wadeni wetu.
13 [j]Usitutie majaribuni,
bali utuokoe kutoka kwa yule
mwovu
[kwa kuwa Ufalme ni wako, na
nguvu,
na utukufu, hata milele. Amen].'

14 [k]Kwa kuwa kama mkiwasamehe watu
wengine wanapowakosea, Baba yenu wa
mbinguni atawasamehe ninyi pia. 15 [l]Lakini
msipowasamehe watu wengine makosa
yao, naye Baba yenu hatawasamehe ninyi
makosa yenu.

*Kuhusu Kufunga*

16 [m]"Mnapofunga, msiwe wenye huzuni
kama wafanyavyo wanafiki. Maana wao
hukunja nyuso zao ili kuwaonyesha
wengine kwamba wamefunga. Amin,
amin nawaambia wao wamekwisha
kupata thawabu yao kamilifu. 17 [n]Lakini
mnapofunga, jipakeni mafuta kichwani na
kunawa nyuso zenu 18 [o]ili kufunga kwenu
kusionekane na watu wengine ila Baba
yenu aketiye mahali pa siri; naye Baba
yenu aonaye sirini atawapa thawabu yenu
kwa wazi.

*Akiba Ya Mbinguni*

**(Luka 12:33-34)**

19 [p]"Msijiwekee hazina duniani, mahali
ambapo nondo na kutu huharibu, nao
wevi huvunja na kuiba. 20 [q]Lakini jiwekeeni
hazina mbinguni, mahali ambapo nondo
na kutu haviharibu, wala wevi hawavunji
na kuiba. 21 [r]Kwa sababu mahali hazina
yako ilipo, hapo ndipo pia moyo wako
utakapokuwa.

*Jicho Ni Taa Ya Mwili*

**(Luka 11:34-36)**

22 [s]"Jicho ni taa ya mwili. Kama jicho
lako ni nyofu, mwili wako wote utajaa nuru.

[a]**6:3** Rum 12:8
[b]**6:4** Mt 6:6, 18; Kol 3:23-24
[c]**6:5** Mk 11:25; Lk 18:10-14
[d]**6:6** 1Fal 4:33
[e]**6:7** Mhu 5:2; 1Fal 18:26-29
[f]**6:8** Mt 6:32
[g]**6:9** Lk 11:2-4; Yn 17:6
[h]**6:11** Mit 30:8
[i]**6:12** Mt 18:21-35
[j]**6:13** Yak 1:13; Mt 5:37
[k]**6:14** Efe 4:32; Kol 3:13
[l]**6:15** Mk 11:25-26; Mt 18:35
[m]**6:16** Isa 58:5-9; Zek 8:19
[n]**6:17** Rut 3:3; Dan 10:3
[o]**6:18** Mt 6:4, 6
[p]**6:19** Mt 23:4; Lk 12:16-21; Yak 5:2-3
[q]**6:20** 1Tim 6:19; Mt 19:20; Lk 12:33-34; Kol 3:1-3
[r]**6:21** Lk 12:34
[s]**6:22** Lk 11:34-36

23 [a]Lakini kama jicho lako ni ovu, mwili
wako wote utajawa na giza. Kwa hiyo basi,
kama nuru iliyomo ndani yako ni giza, hilo
ni giza kuu namna gani!

*Mungu Na Mali*

**(Luka 16:13; 12:22-31)**

24 [b]"Hakuna mtu awezaye kuwatumikia
mabwana wawili. Kwa kuwa atamchukia
huyu na kumpenda yule mwingine, au
atashikamana sana na huyu na kumdharau
yule mwingine. Hamwezi kumtumikia
Mungu pamoja na Mali.[c]

*Msiwe Na Wasiwasi*

25 [d]"Kwa hiyo nawaambia, msisumbukie
maisha yenu kwamba mtakula nini au
mtakunywa nini; au msumbukie miili yenu
kwamba mtavaa nini. Je, maisha si zaidi
ya chakula, na mwili zaidi ya mavazi?
26 [e]Waangalieni ndege wa angani; wao
hawapandi wala hawavuni au kuweka
ghalani, lakini Baba yenu wa mbinguni
huwalisha. Je, ninyi si wa thamani zaidi
kuliko hao ndege? 27 [f]Ni nani miongoni
mwenu ambaye kwa kujitaabisha kwake
anaweza kujiongezea hata saa moja zaidi
katika maisha yake?

28 "Nanyi kwa nini mnajitaabisha kwa
ajili ya mavazi? Fikirini maua ya shambani
yameavyo. Hayafanyi kazi wala hayafumi.
29 [g]Lakini nawaambia, hata Solomoni katika
fahari yake yote hakuvikwa vizuri kama
mojawapo ya hayo maua. 30 [h]Basi ikiwa
Mungu huyavika hivi majani ya shambani,
ambayo leo yapo na kesho yanatupwa
motoni, je, hatawavika ninyi vizuri
zaidi, enyi wa imani haba? 31 Kwa hiyo
msiwe na wasiwasi, mkisema, 'Tutakula
nini?' au 'Tutakunywa nini?' au 'Tutavaa
nini?' 32 [i]Watu wasiomjua Mungu ndio
wanaoshindania hayo, lakini Baba yenu
wa mbinguni anafahamu kuwa mnahitaji
haya yote. 33 [j]Lakini utafuteni kwanza
Ufalme wa Mungu na haki yake, na haya
yote atawapa pia. 34 Kwa hiyo msiwe na
wasiwasi kuhusu kesho, kwa sababu kesho
itajitaabikia yenyewe. Yatosha kwa siku
masumbufu yake.

*Kuwahukumu Wengine*

**(Luka 6:37-38, 41-42)**

7 [k]"Usihukumu ili usije ukahukumiwa.
2 [l]Kwa maana jinsi unavyowahukumu
wengine, ndivyo utakavyohukumiwa,
na kwa kipimo kile upimiacho, ndicho
utakachopimiwa.

3 [m]"Mbona unatazama kibanzi kilicho
ndani ya jicho la ndugu yako, na wala huoni
boriti iliyo ndani ya jicho lako mwenyewe?
4 Au unawezaje kumwambia ndugu yako,
'Acha nitoe kibanzi kwenye jicho lako,'
wakati kuna boriti kwenye jicho lako
mwenyewe? 5 Ewe mnafiki, ondoa boriti
ndani ya jicho lako kwanza, ndipo utaweza
kuona dhahiri jinsi ya kuondoa kibanzi
kilicho ndani ya jicho la ndugu yako.

6 [n]"Msiwape mbwa vitu vilivyo vitakatifu;
wala msitupie nguruwe lulu zenu. Kama
mkifanya hivyo, watazikanyagakanyaga na
kisha watawageukia na kuwararua vipande
vipande.

*Omba, Tafuta, Bisha*

**(Luka 11:9-13)**

7 [o]"Ombeni nanyi mtapewa; tafuteni
nanyi mtapata; bisheni nanyi mtafunguliwa
mlango. 8 [p]Kwa kuwa kila aombaye hupewa;
naye kila atafutaye hupata; na kila abishaye
hufunguliwa mlango.

9 "Au ni nani miongoni mwenu ambaye

---

[a]**6:23** Mt 20:15
[b]**6:24** Lk 16:9, 13
[c]24 Mali (au Utajiri) hapa inatoka neno Mamoni kwa Kiaramu au Mamona kwa Kiyunani.
[d]**6:25** Flp 4:6; 1Pet 5:7
[e]**6:26** Za 104:21; 136:25; Mt 10:29-31
[f]**6:27** Za 39:5
[g]**6:29** 1Fal 10:4-7
[h]**6:30** Mt 16:8; Lk 12:28
[i]**6:32** Mt 6:8
[j]**6:33** Za 37:4, 25; Rum 14:17; Mk 10:29-30
[k]**7:1** 1Kor 5:12; Yak 4:11-12
[l]**7:2** Lk 6:38; Rum 2:1
[m]**7:3** Lk 6:41, 42
[n]**7:6** Mt 9:7, 8; 23:9; Mdo 13:13, 45, 46; Mt 10:11
[o]**7:7** 1Fal 3:5; Mk 11:24; Yer 29:13-14
[p]**7:8** Mit 8:17; 29:12-13

mwanawe akimwomba mkate atampa jiwe?
[10] Au mwanawe akimwomba samaki atampa
nyoka? [11] [a]Ikiwa ninyi basi mlio waovu
mnajua kuwapa watoto wenu vitu vizuri,
si zaidi sana Baba yenu aliye mbinguni
atawapa vitu vizuri wale wamwombao?
[12] [b]Kwa hiyo chochote mnachotaka
mtendewe na watu, ninyi nanyi watendeeni
vivyo hivyo. Kwa kuwa hii ndiyo Sheria
na Manabii.

*Njia Nyembamba Na Njia Pana*

[13] [c]"Ingieni kupitia mlango mwembamba,
kwa maana lango ni pana na njia ni pana
ielekeayo upotevuni, nao ni wengi waingiao
kwa kupitia lango hilo. [14] [d]Lakini mlango
ni mwembamba na njia ni finyu ielekeayo
kwenye uzima, nao ni wachache tu waionao.

*Mti Na Tunda Lake*

**(Luka 6:43-44)**

[15] [e]"Jihadharini na manabii wa uongo,
wanaowajia wakiwa wamevaa mavazi
ya kondoo, lakini ndani ni mbwa mwitu
wakali. [16] [f]Mtawatambua kwa matunda yao.
Je, watu huchuma zabibu kwenye miiba, au
tini kwenye michongoma? [17] [g]Vivyo hivyo,
mti mwema huzaa matunda mazuri, na
mti mbaya huzaa matunda mabaya. [18] [h]Mti
mwema hauwezi kuzaa matunda mabaya,
wala mti mbaya hauwezi kuzaa matunda
mazuri. [19] [i]Kila mti usiozaa matunda mazuri
hukatwa na kutupwa motoni. [20] Hivyo,
mtawatambua kwa matunda yao.

*Mwanafunzi Wa Kweli*

**(Luka 13:25-27)**

[21] [j]"Si kila mtu aniambiaye, 'Bwana,
Bwana,' atakayeingia katika Ufalme wa
Mbinguni, bali ni yeye afanyaye mapenzi
ya Baba yangu aliye mbinguni. [22] [k]Wengi
wataniambia siku ile, 'Bwana, Bwana,
hatukutoa unabii kwa jina lako, na kwa
jina lako kutoa pepo wachafu na kufanya
miujiza mingi?' [23] [l]Ndipo nitakapowaambia
wazi, 'Sikuwajua kamwe. Ondokeni
kwangu, ninyi watenda maovu!'

*Msikiaji Na Mtendaji*

**(Luka 6:47-49)**

[24] [m]"Kwa hiyo kila mtu ayasikiaye haya
maneno yangu na kuyatenda, ni kama mtu
mwenye busara aliyejenga nyumba yake
kwenye mwamba. [25] Mvua ikanyesha,
mafuriko yakaja, na upepo ukavuma
ukaipiga hiyo nyumba. Lakini haikuanguka;
kwa sababu msingi wake ulikuwa kwenye
mwamba. [26] Naye kila anayesikia haya
maneno yangu wala asiyatende, ni kama
mtu mjinga aliyejenga nyumba yake
kwenye mchanga. [27] [n]Mvua ikanyesha,
mafuriko yakaja, nao upepo ukavuma
ukaipiga hiyo nyumba, nayo ikaanguka
kwa kishindo kikubwa."
[28] [o]Yesu alipomaliza kusema maneno
haya, makutano ya watu wakashangazwa
sana na mafundisho yake, [29] [p]kwa sababu
alifundisha kama yeye aliye na mamlaka,
wala si kama walimu wao wa sheria.

*Yesu Amtakasa Mwenye Ukoma*

**(Marko 1:40-45; Luka 5:12-16)**

8 Yesu aliposhuka kutoka mlimani,
makutano makubwa ya watu
yakamfuata. [2] [q]Mtu mmoja mwenye ukoma
akaja na kupiga magoti mbele yake,
akasema, "Bwana, kama ukitaka, unaweza
kunitakasa."
[3] Yesu akanyoosha mkono wake
akamgusa yule mtu, akamwambia, "Nataka.
Takasika!" Mara yule mtu akatakasika

[a]**7:11** Yak 1:17
[b]**7:12** Lk 6:31; Rum 13:8-10; Gal 5:14
[c]**7:13** Lk 13:24; Yn 10:7-9
[d]**7:14** Mt 19:24; Mdo 14:22
[e]**7:15** Yer 23:16; Mk 13:22; Eze 22:27; Mdo 20:29; Isa 1:23
[f]**7:16** Mt 12:33; Lk 6:44
[g]**7:17** Mt 12:33
[h]**7:18** Lk 6:43
[i]**7:19** Mt 3:10
[j]**7:21** Hos 8:2; Yn 13:13; Yak 1:22; 1Yn 3:18; Rum 2:13
[k]**7:22** Mt 10:15; Lk 10:20; Mdo 19:13
[l]**7:23** Za 6:8; Lk 13:25-27
[m]**7:24** Mt 7:21; Yak 1:22-25
[n]**7:27** Eze 13:10, 11
[o]**7:28** Mt 19:1; 26:1; Mk 11:18; Yn 7:46
[p]**7:29** Yn 7:46
[q]**8:2** Law 13:45; Lk 17:12; Mt 18:26; 20:22

ukoma wake. 4 [a]Kisha Yesu akamwambia,
“Hakikisha humwambii mtu yeyote. Lakini
nenda ukajionyeshe kwa kuhani, na utoe
sadaka aliyoamuru Mose, ili kuwa ushuhuda
kwao.”

*Yesu Amponya Mtumishi Wa Jemadari*

**(Luka 7:1-10)**

5 [b]Yesu alipoingia Kapernaumu, jemadari
mmoja alimjia, kumwomba msaada,
6 [c]akisema, “Bwana, mtumishi wangu
amelala nyumbani na amepooza, tena ana
maumivu makali ya kutisha.”

7 Yesu akamwambia, “Nitakuja na
kumponya.”

8 [d]Lakini yule jemadari akamwambia,
“Bwana, mimi sistahili wewe kuingia chini
ya dari yangu. Lakini sema neno tu, naye
mtumishi wangu atapona. 9 Kwa kuwa mimi
mwenyewe ni mtu niliyewekwa chini ya
mamlaka, nikiwa na askari chini yangu.
Nikimwambia huyu, ‘Nenda,’ yeye huenda;
na mwingine nikimwambia, ‘Njoo,’ yeye
huja. Nikimwambia mtumishi wangu,
‘Fanya hivi,’ yeye hufanya.”

10 [e]Yesu aliposikia maneno haya,
alishangaa, akawaambia wale waliomfuata,
“Amin, nawaambia, hata katika Israeli
sijapata kuona yeyote mwenye imani
kubwa namna hii. 11 [f]Ninawaambia kwamba
wengi watatoka mashariki na magharibi,
nao wataketi karamuni pamoja na
Abrahamu, Isaki na Yakobo katika Ufalme
wa Mbinguni. 12 [g]Lakini warithi wa Ufalme
watatupwa katika giza la nje, ambako
kutakuwako kilio na kusaga meno.”

13 [h]Kisha Yesu akamwambia yule
jemadari, “Nenda na iwe kwako sawasawa
na imani yako.” Naye yule mtumishi
akapona saa ile ile.

*Yesu Aponya Wengi*

**(Marko 1:29-34; Luka 4:38-41)**

14 [i]Yesu alipoingia nyumbani kwa Petro,
alimkuta mama mkwe wa Petro amelala
kitandani, akiwa ana homa. 15 [j]Akamgusa
mkono wake na homa ikamwacha, naye
akainuka na kuanza kumhudumia.

16 [k]Jioni ile, wakamletea watu wengi
waliopagawa na pepo wachafu, naye
akawatoa wale pepo wachafu kwa neno lake,
na kuwaponya wagonjwa wote. 17 [l]Haya
yalifanyika ili litimie lile lililonenwa kwa
kinywa cha nabii Isaya kwamba:

“Mwenyewe alitwaa udhaifu wetu
na alichukua magonjwa yetu.”

*Gharama Ya Kumfuata Yesu*

**(Luka 9:57-62)**

18 [m]Yesu alipoona makutano mengi
wamemzunguka, aliwaamuru wanafunzi
wake wavuke mpaka ng’ambo ya ziwa.
19 [n]Kisha mwalimu mmoja wa sheria
akamjia Yesu na kumwambia, “Mwalimu,
nitakufuata kokote uendako.”

20 [o]Naye Yesu akamjibu, “Mbweha wana
mapango, nao ndege wa angani wana viota,
lakini Mwana wa Adamu hana mahali pa
kulaza kichwa chake.”

21 [p]Mwanafunzi mwingine akamwambia,
“Bwana, niruhusu kwanza nikamzike baba
yangu.”

22 [q]Lakini Yesu akamwambia, “Nifuate,
uwaache wafu wawazike wafu wao.”

*Yesu Atuliza Dhoruba*

**(Marko 4:35-41; Luka 8:22-25)**

23 [r]Naye alipoingia kwenye mashua,
wanafunzi wake wakamfuata. 24 [s]Ghafula,
kukainuka dhoruba kali baharini hata

[a]**8:4** Mk 8:30; Lk 4:41; Law 14:2-32
[b]**8:5** Lk 7:1; Yn 4:27
[c]**8:6** Mt 4:24
[d]**8:8** Za 107:20
[e]**8:10** Mt 15:28
[f]**8:11** Za 107:3; Mal 1:11; Lk 13:29
[g]**8:12** Mt 13:38; 25:30; Lk 13:28
[h]**8:13** Mt 9:22-29
[i]**8:14** 1Kor 9:5
[j]**8:15** Mk 1:29-34
[k]**8:16** Mt 4:23-24
[l]**8:17** Isa 53:4; Mt 1:22
[m]**8:18** Mk 4:35; Lk 8:22
[n]**8:19** Lk 9:57, 58
[o]**8:20** Dan 7:13; Mk 2:10
[p]**8:21** 1Fal 19:20
[q]**8:22** Mt 4:19; Rum 6:13
[r]**8:23** Za 4:8
[s]**8:24** Mk 4:37; Lk 8:26

mashua ikaanza kufunikwa na mawimbi,
lakini Yesu alikuwa amelala usingizi.
25 Wanafunzi wake wakamwendea na
kumwamsha, wakisema, “Bwana, tuokoe!
Tunazama!”
26 [a]Naye Yesu akawaambia, “Kwa nini
mnaogopa, enyi wa imani haba?” Kisha
akaamka na kukemea dhoruba na mawimbi,
nako kukawa shwari kabisa.
27 Wale watu wakashangaa, wakisema,
“Ni mtu wa namna gani huyu? Hata upepo
na mawimbi vinamtii!”

*Wawili Wenye Pepo Waponywa*

**(Marko 5:1-20; Luka 8:26-39)**

28 [b]Walipofika ng’ambo katika nchi ya
Wagerasi, watu wawili waliopagawa na
pepo wachafu walitoka makaburini nao
wakakutana naye. Watu hawa walikuwa
wakali mno kiasi kwamba hakuna mtu
aliyeweza kupita njia ile. 29 [c]Wakapiga
kelele, “Una nini nasi, Mwana wa Mungu?
Umekuja hapa kututesa kabla ya wakati
ulioamriwa?”
30 Mbali kidogo kutoka pale walipokuwa,
kulikuwa na kundi kubwa la nguruwe
wakilisha. 31 Wale pepo wachafu wakamsihi
Yesu, “Ukitutoa humu, turuhusu twende
kwenye lile kundi la nguruwe.”
32 Akawaambia, “Nendeni!” Hivyo
wakatoka na kuwaingia wale nguruwe, nalo
kundi lote likateremka gengeni kwa kasi,
likaingia katika ziwa na kufa ndani ya maji.
33 Wale watu waliokuwa wakiwachunga hao
nguruwe wakakimbia wakaingia mjini,
wakaeleza yote kuhusu yale yaliyowatokea
wale waliokuwa wamepagawa na pepo
wachafu. 34 [d]Kisha watu wote wa mji huo
wakatoka kwenda kukutana na Yesu. Nao
walipomwona wakamsihi aondoke kwenye
nchi yao.

[a]**8:26** Mt 6:30; Za 65:7; 89:9
[b]**8:28** Mt 4:24
[c]**8:29** Lk 4:34; 2Pet 2:4
[d]**8:34** Lk 5:8; Mdo 16:39

*Yesu Amponya Mtu Aliyepooza*

**(Marko 2:1-12; Luka 5:17-26)**

9 [e]Yesu akaingia kwenye chombo, akavuka
na kufika katika mji wa kwao. 2 [f]Wakati
huo huo wakamletea mtu aliyepooza,
akiwa amelazwa kwenye mkeka. Yesu
alipoiona imani yao, alimwambia yule mtu
aliyepooza, “Mwanangu, jipe moyo mkuu.
Dhambi zako zimesamehewa.”
3 [g]Kwa ajili ya jambo hili, baadhi ya
walimu wa sheria wakasema mioyoni
mwao, “Huyu mtu anakufuru!”
4 [h]Lakini Yesu akiyafahamu mawazo
yao, akawaambia, “Kwa nini mnawaza
maovu mioyoni mwenu? 5 Je, ni lipi lililo
rahisi zaidi: kusema, ‘Umesamehewa
dhambi zako,’ au kusema, ‘Inuka, uende’?
6 [i]Lakini, ili mpate kujua kwamba Mwana
wa Adamu anayo mamlaka duniani
kusamehe dhambi…” Ndipo akamwambia
yule aliyepooza, “Inuka, chukua mkeka
wako, uende nyumbani kwako.” 7 Yule
mtu akasimama, akaenda nyumbani kwake.
8 [j]Makutano walipoyaona haya, wakajawa
na hofu ya Mungu, wakamtukuza Mungu
ambaye alikuwa ametoa mamlaka kama
haya kwa wanadamu.

*Kuitwa Kwa Mathayo*

**(Marko 2:13-17; Luka 5:27-32)**

9 [k]Yesu alipokuwa akienda kutoka huko,
alimwona mtu mmoja jina lake Mathayo
akiwa ameketi forodhani mahali pa kutoza
ushuru. Yesu akamwambia, “Nifuate.”
Mathayo akaondoka, akamfuata.
10 Yesu alipokuwa akila chakula ndani ya
nyumba ya Mathayo, watoza ushuru wengi
na “wenye dhambi” wakaja kula pamoja
naye na wanafunzi wake. 11 [l]Mafarisayo
walipoona mambo haya, wakawauliza
wanafunzi wake, “Kwa nini Mwalimu

[e]**9:1** Mt 4:13
[f]**9:2** Mt 4:24; 9:22; Yn 16:33; Lk 7:48
[g]**9:3** Mt 26:65; Yn 10:33; Mk 2:7
[h]**9:4** Za 94:11; Yn 2:22
[i]**9:6** Mt 9:22
[j]**9:8** Yn 15:8; Mdo 4:21
[k]**9:9** Mt 4:19
[l]**9:11** Lk 19:7; Gal 2:15

wenu anakula pamoja na watoza ushuru
na 'wenye dhambi'?"
12 Lakini Yesu aliposikia hayo,
akawaambia, "Watu wenye afya hawahitaji
tabibu, lakini wale walio wagonjwa ndio
wanaohitaji tabibu. 13 [a]Nendeni mkajifunze
maana ya maneno haya: 'Nataka rehema,
wala si dhabihu.' Kwa maana sikuja kuwaita
wenye haki, bali wenye dhambi."

### *Yesu Aulizwa Kuhusu Kufunga*

**(Marko 2:18-22; Luka 5:33-39)**

14 [b]Wanafunzi wa Yohana Mbatizaji
wakaja na kumuuliza Yesu, "Imekuwaje
kwamba sisi na Mafarisayo tunafunga,
lakini wanafunzi wako hawafungi?"
15 [c]Yesu akawajibu, "Wageni wa bwana
arusi wawezaje kuomboleza wakati angali
pamoja nao? Wakati utafika ambapo bwana
arusi ataondolewa kwao. Hapo ndipo
watakapofunga.
16 [d]"Hakuna mtu anayeshonea kiraka
kipya kwenye nguo iliyochakaa, kwa maana
kile kiraka kitachanika kutoka kwenye hiyo
nguo, nayo hiyo nguo itachanika zaidi.
17 Wala watu hawaweki divai mpya kwenye
viriba vikuukuu. Kama wakifanya hivyo,
viriba vitapasuka nayo divai itamwagika,
navyo viriba vitaharibika. Lakini divai
mpya huwekwa kwenye viriba vipya, na
hivyo divai na viriba huwa salama."

### *Mwanamke Aponywa*

**(Marko 5:21-43; Luka 8:40-56)**

18 [e]Yesu alipokuwa akiwaambia mambo
haya, mara akaingia kiongozi wa sinagogi
akapiga magoti mbele yake, akamwambia,
"Binti yangu amekufa sasa hivi. Lakini njoo
uweke mkono wako juu yake, naye atakuwa
hai." 19 Yesu akaondoka akafuatana naye,
nao wanafunzi wake pia wakaandamana
naye.
20 [f]Wakati huo huo, mwanamke mmoja,
ambaye alikuwa na ugonjwa wa kutokwa
damu kwa muda wa miaka kumi na miwili,
akaja nyuma ya Yesu, akagusa upindo wa
vazi lake, 21 [g]kwa maana alisema moyoni
mwake, "Kama nikigusa tu vazi lake,
nitaponywa."
22 [h]Yesu akageuka, naye alipomwona
akamwambia, "Binti, jipe moyo mkuu,
imani yako imekuponya." Naye yule
mwanamke akapona kuanzia saa ile ile.

### *Yesu Amfufua Binti Wa Kiongozi Wa Sinagogi*

23 [i]Yesu alipofika nyumbani kwa
yule kiongozi wa sinagogi na kuwaona
waombolezaji wakipiga filimbi za
maombolezo na watu wengi wakipiga
kelele, 24 [j]akawaambia, "Ondokeni! Kwa
maana binti huyu hakufa, bali amelala."
Wakamcheka kwa dhihaka. 25 [k]Lakini watu
walipokwisha kutolewa nje, akaingia mle
ndani na kumshika yule binti mkono, naye
akaamka. 26 [l]Habari hizi zikaenea katika
maeneo yale yote.

### *Yesu Awaponya Vipofu*

27 [m]Yesu alipokuwa akiondoka mahali
pale, vipofu wawili wakamfuata wakipiga
kelele kwa nguvu na kusema, "Mwana wa
Daudi, tuhurumie!"
28 [n]Alipoingia mle nyumbani wale
vipofu wakamjia. Naye Yesu akawauliza,
"Mnaamini kwamba ninaweza kufanya
jambo hili?"

Wakamjibu, "Ndiyo, Bwana."
29 [o]Ndipo Yesu akagusa macho yao na
kusema, "Iwe kwenu sawasawa na imani
yenu." 30 [p]Macho yao yakafunguka. Yesu
akawaonya vikali, akisema, "Angalieni mtu

---

[a]**9:13** Mik 6:6-8; Mt 12:7; Lk 19:10; 1Tim 1:15
[b]**9:14** Mt 11:18-19; Lk 18:12
[c]**9:15** Yn 3:29; Mdo 13:2-3; 14:23
[d]**9:16** Yn 1:17
[e]**9:18** Mt 8:2; Mk 5:23
[f]**9:20** Mk 6:56; Lk 6:19
[g]**9:21** Mt 14:36
[h]**9:22** Lk 17:19; 18:42; Mt 15:28
[i]**9:23** 2Nya 35:25; Yer 9:17-18
[j]**9:24** Mdo 20:10; Dan 12:2; 1The 4:13-16; Yn 11:11
[k]**9:25** Lk 7:14
[l]**9:26** Mk 1:28, 45; Lk 5:15
[m]**9:27** Mk 10:47; Lk 18:38-39
[n]**9:28** Mdo 14:19
[o]**9:29** Mt 8:11; 9:22
[p]**9:30** Mt 8:4

yeyote asijue kuhusu jambo hili.” [31] [a]Lakini
wao wakaenda na kueneza habari zake
katika eneo lile lote.

*Yesu Amponya Mtu Bubu*

[32] [b]Walipokuwa wanatoka, mtu mmoja
aliyekuwa amepagawa na pepo mchafu na
ambaye hakuweza kuongea aliletwa kwa
Yesu. [33] [c]Yule pepo mchafu alipotolewa,
yule mtu aliyekuwa bubu akaongea. Ule
umati wa watu ukastaajabu na kusema,
“Jambo kama hili kamwe halijapata
kuonekana katika Israeli.”
[34] [d]Lakini Mafarisayo wakasema, “Huyo
anatoa pepo wachafu kwa uwezo wa mkuu
wa pepo wachafu.”

*Watendakazi Ni Wachache*

[35] [e]Yesu akazunguka katika miji yote na
vijiji vyote, akifundisha katika masinagogi
yao, akihubiri habari njema za Ufalme,
na akiponya kila ugonjwa na kila aina
ya maradhi. [36] [f]Alipoona makutano,
aliwahurumia kwa sababu walikuwa
wanasumbuka bila msaada, kama kondoo
wasiokuwa na mchungaji. [37] [g]Ndipo
akawaambia wanafunzi wake, “Mavuno
ni mengi lakini watendakazi ni wachache.
[38] [h]Kwa hiyo mwombeni Bwana wa mavuno,
ili apeleke watendakazi katika shamba lake
la mavuno.”

*Yesu Awatuma Wale Kumi Na Wawili*

**(Marko 3:13-19; 6:7-13; Luka 6:12-16; 9:1-6)**

10 [i]Ndipo Yesu akawaita wanafunzi
wake kumi na wawili, naye akawapa
mamlaka juu ya pepo wachafu, ili waweze
kuwatoa na kuponya kila ugonjwa na
maradhi ya kila aina.
[2] [j]Haya ndiyo majina ya hao mitume kumi
na wawili: wa kwanza, Simoni aitwaye
Petro, na Andrea nduguye; Yakobo mwana
wa Zebedayo, na Yohana nduguye; [3] Filipo,
na Bartholomayo; Tomaso, na Mathayo
mtoza ushuru; Yakobo mwana wa Alfayo,
na Thadayo; [4] [k]Simoni Mkananayo, na Yuda
Iskariote aliyemsaliti Yesu.
[5] [l]Hawa kumi na wawili, Yesu aliwatuma
akawaagiza: “Msiende miongoni mwa watu
wa Mataifa, wala msiingie mji wowote wa
Wasamaria. [6] [m]Lakini afadhali mshike njia
kuwaendea kondoo wa nyumba ya Israeli
waliopotea. [7] [n]Wakati mnapokwenda,
hubirini mkisema, ‘Ufalme wa Mbinguni
umekaribia.’ [8] [o]Ponyeni wagonjwa, fufueni
wafu, takaseni wenye ukoma, toeni pepo
wachafu. Mmepata bure, toeni bure.
[9] [p]Msichukue dhahabu, wala fedha, wala
shaba kwenye vifuko vyenu. [10] [q]Msichukue
mkoba wa safari, wala kanzu mbili, wala
jozi ya pili ya viatu, wala fimbo, kwa maana
mtendakazi anastahili posho yake.
[11] [r]“Mji wowote au kijiji chochote
mtakapoingia, tafuteni humo mtu
anayestahili, nanyi kaeni kwake mpaka
mtakapoondoka. [12] [s]Mkiingia kwenye
nyumba, itakieni amani. [13] [t]Kama nyumba
hiyo inastahili, amani yenu na iwe juu yake.
La sivyo, amani yenu na iwarudie ninyi.
[14] [u]Kama mtu yeyote hatawakaribisha ninyi,
wala kusikiliza maneno yenu, kung’uteni
mavumbi kutoka kwenye miguu yenu
mtakapokuwa mnatoka kwenye nyumba
hiyo au mji huo. [15] [v]Amin, nawaambia,
itakuwa rahisi zaidi kwa miji ya Sodoma na

[a]**9:31** Mt 9:26; Mk 7:36
[b]**9:32** Mt 4:24; 12:22-24
[c]**9:33** Mk 2:12
[d]**9:34** Mt 12:24
[e]**9:35** Mt 4:23
[f]**9:36** Mt 15:32; Mk 8:2; 6:34; 1Fal 22:17
[g]**9:37** Yn 4:35; Lk 10:2
[h]**9:38** 2The 3:1
[i]**10:1** Mk 3:13-15; Lk 9:1-5
[j]**10:2** Lk 6:13-16
[k]**10:4** Mk 14:10; Mdo 1:16
[l]**10:5** 1Fal 16:24; Lk 10:33
[m]**10:6** Yer 50:6; Mt 15:24
[n]**10:7** Mt 3:2; Lk 19:9
[o]**10:8** Mdo 20:33
[p]**10:9** Lk 22:35
[q]**10:10** 1Tim 5:18; Hes 18:31
[r]**10:11** Lk 10:8
[s]**10:12** 1Sam 25:6; Lk 10:5-6
[t]**10:13** Lk 10:5; Za 35:13
[u]**10:14** Neh 5:13; Mk 6:11
[v]**10:15** Mwa 18:20; Yud 7; Mdo 17:30; Mt 11:22-24

Gomora kustahimili katika hukumu kuliko
mji huo.

*Mateso Yanayokuja*

**(Marko 13:9-13; Luka 21:12-17)**

16 [a]"Tazama, ninawatuma kama kondoo
katikati ya mbwa mwitu. Kwa hiyo mwe
werevu kama nyoka na wapole kama hua.
17 [b]"Jihadharini na wanadamu; kwa
maana watawapeleka katika mabaraza
yao na kuwapiga kwenye masinagogi yao.
18 [c]Nanyi mtaburutwa mbele ya watawala na
wafalme kwa ajili yangu, ili kuwa ushuhuda
kwao na kwa watu wa Mataifa. 19 [d]Lakini
watakapowapeleka humo, msisumbuke
kufikiria mtakalosema, kwa maana
mtapewa la kusema wakati huo. 20 [e]Kwa
sababu si ninyi mtakaokuwa mkinena,
bali ni Roho wa Baba yenu atakayekuwa
akinena kupitia kwenu.
21 [f]"Ndugu atamsaliti ndugu yake ili
auawe, naye baba atamsaliti mtoto wake.
Watoto nao wataasi dhidi ya wazazi wao
na kusababisha wauawe. 22 [g]Watu wote
watawachukia kwa ajili ya Jina langu.
Lakini yule atakayevumilia hadi mwisho
ataokolewa. 23 [h]Wakiwatesa katika mji
mmoja, kimbilieni mji mwingine. Amin,
amin nawaambia, hamtamaliza miji yote
ya Israeli kabla Mwana wa Adamu kuja.
24 [i]"Mwanafunzi hawezi kumzidi
mwalimu wake, wala mtumishi hamzidi
bwana wake. 25 [j]Yatosha mwanafunzi kuwa
kama mwalimu wake, na mtumishi kuwa
kama bwana wake. Ikiwa mkuu wa nyumba
ameitwa Beelzebuli,[k] je, si watawaita zaidi
wale wa nyumbani mwake!

*Anayestahili Kuogopwa*

**(Luka 12:2-9)**

26 [l]"Kwa hiyo msiwaogope hao, kwa
maana hakuna kilichofichika ambacho
hakitafunuliwa, wala hakuna siri ambayo
haitajulikana. 27 Ninalowaambia gizani,
ninyi lisemeni mchana peupe. Na lile
mnalosikia likinong'onwa masikioni
mwenu, lihubirini juu ya nyumba.
28 [m]Msiwaogope wale wauao mwili lakini
hawawezi kuua roho. Afadhali mwogopeni
yeye awezaye kuiangamiza roho na mwili
katika jehanamu.[n] 29 Je, shomoro wawili
hawauzwi kwa senti moja tu? Lakini hakuna
hata mmoja wao atakayeanguka chini
pasipo Baba yenu kujua. 30 [o]Hata nywele za
vichwa vyenu zote zimehesabiwa. 31 [p]Hivyo
msiogope; kwa maana ninyi ni wa thamani
kubwa kuliko shomoro wengi.
32 [q]"Kila mtu atakayenikiri mbele ya watu,
mimi nami nitamkiri yeye mbele za Baba
yangu aliye mbinguni. 33 [r]Lakini yeyote
atakayenikana mimi mbele ya watu, mimi
nami nitamkana mbele za Baba yangu aliye
mbinguni."

*Sikuleta Amani, Bali Upanga*

**(Luka 12:51-53; 14:26-27)**

34 [s]"Msidhani kwamba nimekuja kuleta
amani duniani. Sikuja kuleta amani bali
upanga. 35 [t]Kwa maana nimekuja kumfitini

" 'mtu na babaye,
binti na mamaye,
mkwe na mama mkwe wake;
36 [u]nao adui za mtu watakuwa
ni wale watu wa nyumbani
kwake.'

[a]**10:16** Lk 10:3; Mdo 20:29; Rum 16:19; 1Kor 14:20
[b]**10:17** Mt 5:22; Mdo 22:19; 26:11
[c]**10:18** Mdo 25:24-26
[d]**10:19** Kut 4:12; Lk 12:11-12
[e]**10:20** Mdo 4:8; Yn 14:26
[f]**10:21** Mik 7:6; Mt 10:35-36
[g]**10:22** Lk 21:19; Ufu 2:10
[h]**10:23** Mt 16:28; Lk 17:30
[i]**10:24** Lk 6:40; Yn 15:20
[j]**10:25** Mk 3:22; Mt 12:24
[k]25 Beelzebuli kwa Kiyunani ni Beelzebubu, yaani mkuu wa pepo wachafu.
[l]**10:26** Mk 4:22; Lk 8:17
[m]**10:28** Isa 8:12-13; Ebr 10:31
[n]28 Jehanamu kwa Kiyunani ni Gehena, maana yake ni Kuzimu, yaani motoni.
[o]**10:30** 1Fal 1:52; Lk 21:18
[p]**10:31** Mt 6:26; 12:12
[q]**10:32** Rum 10:9
[r]**10:33** Mk 8:38; 2Tim 2:12
[s]**10:34** Lk 12:51-53
[t]**10:35** Mik 7:6
[u]**10:36** Mik 6:7

37 [a]“Yeyote ampendaye baba yake
au mama yake kuliko anavyonipenda
mimi, hastahili kuwa wangu. Yeyote
ampendaye mwanawe au binti yake
kuliko anavyonipenda mimi, hastahili
kuwa wangu. 38 [b]Tena yeyote asiyeuchukua
msalaba wake na kunifuata, hastahili kuwa
wangu. 39 [c]Kwa maana yeyote anayetaka
kuyaokoa maisha yake atayapoteza, lakini
yeyote atakayeyapoteza maisha yake kwa
ajili yangu atayapata.

### *Watakaopokea Thawabu*

**(Marko 9:41)**

40 [d]“Mtu yeyote atakayewapokea
ninyi atakuwa amenipokea mimi, na
yeyote atakayenipokea mimi atakuwa
amempokea yeye aliyenituma. 41 [e]Mtu
yeyote anayempokea nabii kwa kuwa ni
nabii atapokea thawabu ya nabii, naye mtu
anayempokea mwenye haki kwa kuwa ni
mwenye haki atapokea thawabu ya mwenye
haki. 42 [f]Kama yeyote akimpa hata kikombe
cha maji baridi mmoja wa hawa wadogo
kwa kuwa ni mwanafunzi wangu, amin,
nawaambia, hataikosa thawabu yake.”

### *Yesu Na Yohana Mbatizaji*

**(Luka 7:18-35)**

11 [g]Baada ya Yesu kumaliza kutoa
maagizo kwa wanafunzi wake kumi na
wawili, aliondoka hapo akaenda kufundisha
na kuhubiri katika miji yao.

2 [h]Yohana aliposikia akiwa gerezani
mambo ambayo Kristo[i] alikuwa akiyafanya,
aliwatuma wanafunzi wake 3 [j]ili
wakamuulize, “Wewe ndiye yule aliyekuwa
aje, au tumngojee mwingine?”

4 Yesu akajibu, “Rudini mkamwambie
Yohana yale mnayosikia na kuyaona:
5 [k]Vipofu wanapata kuona, viwete
wanatembea, wenye ukoma wanatakaswa,
viziwi wanasikia, wafu wanafufuliwa, na
maskini wanahubiriwa habari njema.
6 [l]Amebarikiwa mtu yule asiyechukizwa
na mimi.”

7 [m]Wale wanafunzi wa Yohana
walipokuwa wanaondoka, Yesu akaanza
kusema na makutano kuhusu Yohana
Mbatizaji. Akawauliza, “Mlipokwenda
kule nyikani, mlikwenda kuona nini? Je,
ni unyasi ukipeperushwa na upepo? 8 Kama
sivyo, mlikwenda kuona nini basi? Mtu
aliyevaa mavazi ya kifahari? La hasha, watu
wanaovaa mavazi ya kifahari wako katika
majumba ya wafalme. 9 [n]Basi mlikwenda
kuona nini? Mlikwenda kumwona nabii?
Naam, nawaambia, yeye ni zaidi ya
nabii. 10 [o]Huyu ndiye ambaye habari zake
zimeandikwa:

> “ ‘Tazama nitamtuma mjumbe wangu
> mbele yako,
> atakayetengeneza njia mbele
> yako.’

11 [p]Amin, nawaambia, miongoni mwa wale
waliozaliwa na wanawake, hajatokea mtu
aliye mkuu kuliko Yohana Mbatizaji. Lakini
aliye mdogo kabisa katika Ufalme wa
Mbinguni ni mkuu kuliko Yohana. 12 [q]Tangu
siku za Yohana Mbatizaji hadi sasa, Ufalme
wa Mbinguni hupatikana kwa nguvu, nao
wenye nguvu wanauteka. 13 [r]Kwa maana
manabii wote na Sheria walitabiri mpaka
wakati wa Yohana. 14 [s]Ikiwa mko tayari
kukubali hilo, yeye ndiye yule Eliya ambaye
manabii walikuwa wamesema angekuja.
15 [t]Yeye aliye na masikio, na asikie.

---

[a]**10:37** Lk 14:26
[b]**10:38** Mt 16:24-25; Lk 14:27
[c]**10:39** Lk 17:33; Yn 12:44
[d]**10:40** Kut 16:8; Gal 4:14; Lk 10:16; Yn 12:44
[e]**10:41** 1Fal 17:10; 18:4; 2Fal 4:8
[f]**10:42** Mt 25:40; Mdo 10:4; Mit 14:30; Mk 9:41
[g]**11:1** Mt 7:28; 26:1
[h]**11:2** Mt 14:3
[i]2 *Kristo* maana yake ni *Masiya,* yaani *Aliyetiwa mafuta.*
[j]**11:3** Za 118:26; Ebr 10:37
[k]**11:5** Lk 4:18-19; Isa 61:1-2
[l]**11:6** Mt 13:21; 26:31
[m]**11:7** Mt 3:1-5
[n]**11:9** Lk 1:76; 7:26
[o]**11:10** Mal 3:1; Lk 7:27
[p]**11:11** Mt 13:17
[q]**11:12** Lk 16:16; 13:24
[r]**11:13** Lk 16:16
[s]**11:14** Mal 4:5; Yn 1:21
[t]**11:15** Lk 14:35; Ufu 2:7

16 [a]“Lakini kizazi hiki nikifananishe
na nini? Kinafanana na watoto waliokaa
sokoni wakiwaita wenzao na kuwaambia,

17 [b]“ ‘Tuliwapigia filimbi,
lakini hamkucheza;
tuliwaimbia nyimbo za maombolezo,
lakini hamkuomboleza.’

18 [c]Kwa maana Yohana Mbatizaji alikuja,
alikuwa hali wala hanywi, nao wanasema,
‘Yeye ana pepo mchafu.’ 19 [d]Mwana wa
Adamu alikuja akila na kunywa, nao
wanasema, ‘Tazameni huyu mlafi na
mlevi, rafiki wa watoza ushuru na “wenye
dhambi.” ’ Lakini hekima huthibitishwa
kuwa kweli kwa matendo yake.”

*Onyo Kwa Miji Isiyotubu*

**(Luka 10:13-15)**

20 [e]Ndipo Yesu akaanza kushutumu miji
ambamo alifanya miujiza yake mingi
kuliko kwingine, kwa maana watu wake
hawakutubu. 21 [f]“Ole wako, Korazini! Ole
wako Bethsaida! Kwa maana kama miujiza
iliyofanyika kwenu, ingefanyika Tiro na
Sidoni, miji hiyo ingekuwa imetubu zamani
kwa kuvaa magunia na kujipaka majivu.
22 [g]Lakini nawaambia, itakuwa rahisi zaidi
kwa Tiro na Sidoni kustahimili katika
siku ya hukumu, kuliko ninyi. 23 [h]Nawe
Kapernaumu, je, utainuliwa hadi mbinguni?
La hasha, utashushwa mpaka kuzimu.[i]
Miujiza iliyofanyika kwako ingefanyika
huko Sodoma, mji huo ungalikuwepo hadi
leo. 24 [j]Lakini nakuambia kwamba, itakuwa
rahisi zaidi kwa Sodoma kustahimili katika
siku ya hukumu kuliko wewe.”

*Hakuna Amjuaye Baba Ila Mwana*

**(Luka 10:21-22)**

25 [k]Wakati huo Yesu alisema, “Nakuhimidi
Baba, Bwana wa mbingu na nchi, kwa kuwa
umewaficha mambo haya wenye hekima na
wenye elimu, nawe ukawafunulia watoto
wadogo. 26 Naam, Baba, kwa kuwa hivyo
ndivyo ilivyokupendeza.
27 [l]“Nimekabidhiwa vitu vyote na Baba
yangu: Hakuna mtu amjuaye Mwana ila
Baba, wala hakuna amjuaye Baba ila
Mwana na yeyote ambaye Mwana anapenda
kumfunulia.

*Yesu Awaita Waliolemewa Na Mizigo*

28 [m]“Njooni kwangu, ninyi nyote
mnaotaabika na kulemewa na mizigo, nami
nitawapumzisha. 29 [n]Jifungeni nira yangu,
mjifunze kutoka kwangu, kwa maana mimi
ni mpole na mnyenyekevu wa moyo, nanyi
mtapata raha nafsini mwenu. 30 [o]Kwa maana
nira yangu ni laini na mzigo wangu ni
mwepesi.”

*Bwana Wa Sabato*

**(Marko 2:23-28; Luka 6:1-5)**

12 [p]Wakati huo Yesu alipitia kwenye
mashamba ya nafaka siku ya Sabato.
Wanafunzi wake walikuwa na njaa, nao
wakaanza kuvunja masuke ya nafaka na
kuyala. 2 [q]Lakini Mafarisayo walipoona
jambo hili, wakamwambia, “Tazama!
Wanafunzi wako wanafanya jambo lisilo
halali kufanywa siku ya Sabato.”
3 [r]Yesu akawajibu, “Je, hamjasoma
alichofanya Daudi na wenzake walipokuwa
na njaa? 4 [s]Aliingia katika nyumba ya
Mungu, akala mikate iliyowekwa wakfu,
yeye na wenzake, jambo ambalo halikuwa
halali kwao kufanya, isipokuwa makuhani

---

[a]**11:16** Lk 7:31
[b]**11:17** Mit 29:9
[c]**11:18** Mt 3:4; Lk 1:15
[d]**11:19** Mt 9:11
[e]**11:20** Lk 10:11
[f]**11:21** Mk 8:22; Yn 1:44; Yoe 3:4; Mk 3:8; Yn 3:5-9
[g]**11:22** Mt 11:24; 10:15
[h]**11:23** Mt 4:13; Isa 14:13-15
[i]23 *Kuzimu* ni *Mahali pa wafu.*
[j]**11:24** Mt 10:15
[k]**11:25** Lk 23:34; Yn 12:27-28; Mt 13:11; 1Kor 1:26-29
[l]**11:27** Mt 28:18; Yn 3:35; 10:15; 17:25-26
[m]**11:28** Yn 7:37
[n]**11:29** Flp 2:5; 1Yn 2:6; Za 116:7; Yer 6:16
[o]**11:30** 1Yn 5:3
[p]**12:1** Kum 23:25
[q]**12:2** Kut 20:10; Yn 9:6
[r]**12:3** 1Sam 21:1-6
[s]**12:4** Law 24:5-9

peke yao. 5 [a]Au hamjasoma katika Sheria
kwamba siku ya Sabato makuhani
huvunja sheria ya Sabato Hekaluni lakini
hawahesabiwi kuwa na hatia? 6 [b]Nawaambia
wazi kwamba, yeye aliye mkuu kuliko
Hekalu yupo hapa. 7 [c]Kama mngekuwa
mmejua maana ya maneno haya, ‘Nataka
rehema, wala si dhabihu,’ msingewalaumu
watu wasio na hatia, 8 [d]kwa maana Mwana
wa Adamu ndiye Bwana wa Sabato.”

### *Yesu Anamponya Mtu Aliyepooza Mkono*

**(Marko 3:1-6; Luka 6:6-11)**

9 [e]Yesu akaondoka mahali hapo, akaingia
ndani ya sinagogi lao, 10 [f]na huko alikuwepo
mtu aliyepooza mkono. Wakitafuta sababu
ya kumshtaki Yesu, wakamuuliza, “Je, ni
halali kuponya siku ya Sabato?”

11 [g]Yesu akawaambia, “Ni nani miongoni
mwenu, mwenye kondoo wake ambaye
huyo kondoo akitumbukia shimoni siku
ya Sabato hatamtoa? 12 [h]Mtu ana thamani
kubwa kuliko kondoo. Kwa hiyo ni halali
kutenda mema siku ya Sabato.”

13 Ndipo akamwambia yule mtu,
“Nyoosha mkono wako.” Akaunyoosha,
nao ukaponywa ukawa mzima kama ule
mwingine. 14 [i]Lakini Mafarisayo wakatoka
nje, wakafanya shauri baya juu ya Yesu
jinsi watakavyoweza kumuua.

### *Mtumishi Aliyechaguliwa Na Mungu*

15 [j]Lakini Yesu alipoyatambua mawazo
yao, akaondoka mahali hapo. Watu wengi
wakamfuata, naye akawaponya wagonjwa
wao wote, 16 [k]akiwakataza wasiseme yeye
ni nani. 17 [l]Hii ilikuwa ili litimie lile neno
lililonenwa kwa kinywa cha nabii Isaya
kusema:

18 [m]“Tazama mtumishi wangu
niliyemchagua,
mpendwa wangu, ninayependezwa
naye.
Nitaweka Roho wangu juu yake,
naye atatangaza haki kwa mataifa.
19 Hatagombana wala hatapiga kelele,
wala hakuna atakayesikia sauti
yake njiani.
20 Mwanzi uliopondeka hatauvunja,
na utambi unaofuka moshi
hatauzima,
mpaka atakapoifanya haki ishinde.
21 [n]Katika Jina lake mataifa
wataweka tumaini lao.”

### *Yesu Na Beelzebuli*

**(Marko 3:20-30; Luka 11:14-23)**

22 [o]Kisha wakamletea mtu aliyekuwa
amepagawa na pepo mchafu, na alikuwa
kipofu na bubu. Yesu akamponya, hata
akaweza kusema na kuona. 23 [p]Watu wote
wakashangaa na kusema, “Je, yawezekana
huyu ndiye Mwana wa Daudi?”

24 [q]Lakini Mafarisayo waliposikia jambo
hili wakasema, “Mtu huyu anatoa pepo
wachafu kwa uwezo wa Beelzebuli,[r] mkuu
wa pepo wachafu.”

25 [s]Yesu alijua walichokuwa wakiwaza,
hivyo akawaambia, “Kila ufalme
ukigawanyika dhidi yake wenyewe
huangamia. Hali kadhalika kila mji au
watu wa nyumba moja waliogawanyika
dhidi yao wenyewe hawawezi kusimama.
26 [t]Kama Shetani akimtoa Shetani, atakuwa
amegawanyika yeye mwenyewe. Basi
ufalme wake utawezaje kusimama? 27 [u]Nami
kama natoa pepo wachafu kwa nguvu za
Beelzebuli, watu wenu je, wao hutoa pepo

---

[a] **12:5** Hes 28:9-10; Yn 7:22-23
[b] **12:6** Mt 12:41-42
[c] **12:7** Hos 6:6; Mt 9:13
[d] **12:8** Mt 8:20
[e] **12:9** Mk 3:1; Lk 6:6
[f] **12:10** Lk 14:3; Yn 9:6
[g] **12:11** Lk 15:5
[h] **12:12** Mt 6:26; 10:31
[i] **12:14** Mwa 37:18; Yn 11:53
[j] **12:15** Mt 4:23
[k] **12:16** Mt 8:4
[l] **12:17** Isa 42:1-4; 41:9
[m] **12:18** Mt 3:7; Isa 42:1-4; 41:9
[n] **12:21** Isa 42:1-4
[o] **12:22** Mt 4:24; 9:32-33
[p] **12:23** Mt 9:27
[q] **12:24** Mk 3:22; Mt 9:34
[r] 24 Beelzebuli au Beelzebubu; pia 12:27.
[s] **12:25** Mt 9:4
[t] **12:26** Mt 4:10
[u] **12:27** Mdo 19:13

wachafu kwa uwezo wa nani? Hivyo basi, wao ndio watakaowahukumu. 28 [a]Lakini kama mimi ninatoa pepo wachafu kwa Roho wa Mungu, basi Ufalme wa Mungu umekuja juu yenu.

29 [b]“Au tena, mtu awezaje kuingia katika nyumba ya mtu mwenye nguvu na kuteka nyara mali zake asipomfunga kwanza yule mwenye nguvu? Akishamfunga, ndipo hakika anaweza kuteka nyara mali zake.

30 [c]“Mtu asiyekuwa pamoja nami yu kinyume nami, na mtu ambaye hakusanyi pamoja nami, hutawanya. 31 [d]Kwa hiyo nawaambia, kila dhambi na kufuru watu watasamehewa, lakini mtu atakayemkufuru Roho Mtakatifu hatasamehewa. 32 [e]Mtu yeyote atakayesema neno dhidi ya Mwana wa Adamu atasamehewa, lakini yeyote anenaye neno dhidi ya Roho Mtakatifu hatasamehewa, iwe katika ulimwengu huu au katika ulimwengu ujao.

*Mti Na Matunda Yake*

**(Luka 6:43-45)**

33 [f]“Ufanye mti kuwa mzuri, nayo matunda yake yatakuwa mazuri. Au ufanye mti kuwa mbaya, na matunda yake yatakuwa mabaya. Kwa maana mti hutambulika kwa matunda yake. 34 [g]Enyi uzao wa nyoka! Mnawezaje kunena mambo mema, wakati ninyi ni waovu? Kwa maana kinywa cha mtu huyanena yale yaliyoujaza moyo wake. 35 [h]Mtu mwema hutoa yaliyo mema kutoka hazina ya mambo mema yaliyohifadhiwa ndani yake, naye mtu mwovu hutoa yaliyo maovu kutoka hazina ya mambo maovu yaliyohifadhiwa ndani yake. 36 Lakini nawaambia, katika siku ya hukumu watu watatoa hesabu kuhusu kila neno lisilo maana walilonena. 37 Kwa maana kwa maneno yako utahesabiwa haki, na kwa maneno yako utahukumiwa.”

*Ishara Ya Yona*

**(Marko 8:11-12; Luka 11:29-32)**

38 [i]Kisha baadhi ya Mafarisayo na walimu wa sheria wakamwambia, “Mwalimu, tunataka kuona ishara kutoka kwako.”

39 [j]Lakini yeye akawajibu, “Kizazi kiovu na cha uzinzi kinaomba ishara! Lakini hakitapewa ishara yoyote isipokuwa ile ishara ya nabii Yona. 40 [k]Kwa maana kama vile Yona alivyokuwa ndani ya tumbo la nyangumi[l] kwa siku tatu, usiku na mchana, vivyo hivyo Mwana wa Adamu atakuwa katika moyo wa nchi siku tatu, usiku na mchana. 41 [m]Siku ya hukumu watu wa Ninawi watasimama pamoja na kizazi hiki na kukihukumu; kwa maana wao walitubu waliposikia mahubiri ya Yona. Na tazama, hapa yupo yeye aliye mkuu kuliko Yona. 42 [n]Malkia wa Kusini atasimama wakati wa hukumu na kukihukumu kizazi hiki. Kwa kuwa yeye alikuja kutoka miisho ya dunia ili kuisikiliza hekima ya Solomoni. Na hapa yupo aliye mkuu kuliko Solomoni.”

*Mafundisho Kuhusu Pepo Mchafu*

**(Luka 11:24-26)**

43 “Pepo mchafu amtokapo mtu, hutangatanga katika sehemu zisizo na maji akitafuta mahali pa kupumzika, lakini hapati. 44 Ndipo husema, ‘Nitarudi kwenye nyumba yangu nilikotoka.’ Naye arudipo huikuta ile nyumba ikiwa tupu, imefagiliwa na kupangwa vizuri. 45 [o]Kisha huenda na kuwaleta pepo wachafu wengine saba wabaya kuliko yeye mwenyewe, nao huingia na kukaa humo. Nayo hali ya mwisho ya yule mtu huwa ni mbaya kuliko ile ya kwanza. Ndivyo itakavyokuwa kwa kizazi hiki kiovu.”

---

[a]**12:28** 1Yn 3:8; Mt 3:2
[b]**12:29** Isa 49:24-25; Lk 11:21-22
[c]**12:30** Mk 9:40; Yn 11:52; Lk 11:23
[d]**12:31** Mk 3:28-29; Lk 12:10
[e]**12:32** Tit 2:12; Efe 1:21; Ebr 6:5
[f]**12:33** Mt 7:16-17; Lk 6:43-44
[g]**12:34** Mt 3:7; 23:33; 15:18; Yn 8:43
[h]**12:35** Lk 6:45
[i]**12:38** Yn 6:30; 1Kor 1:22
[j]**12:39** Yn 1:7; Mt 8:20; 16:21
[k]**12:40** Yn 2:1, 2; 1:17; Mt 8:20; 16:21
[l]40 Nyangumi ni samaki mkubwa sana.
[m]**12:41** Yn 1:2; 3:15
[n]**12:42** 1Fal 10:2; 2Nya 9:1
[o]**12:45** 2Pet 2:20

### *Mama Na Ndugu Zake Yesu*

**(Marko 3:31-35; Luka 8:19-21)**

46 [a]Wakati alikuwa angali anazungumza
na makutano, mama yake na ndugu
zake wakasimama nje wakitaka kuongea
naye. 47 Ndipo mtu mmoja akamwambia,
“Tazama, mama yako na ndugu zako
wamesimama nje, wanataka kuongea na
wewe.”

48 [b]Lakini yeye akamjibu na kumwambia
yule mtu, “Mama yangu ni nani, nao ndugu
zangu ni nani?” 49 Akawanyooshea mkono
wanafunzi wake, akasema, “Hawa hapa
ndio mama yangu na ndugu zangu! 50 [c]Kwa
maana yeyote afanyaye mapenzi ya Baba
yangu wa mbinguni, huyo ndiye ndugu
yangu, na dada yangu na mama yangu.”

### *Mfano Wa Mpanzi*

**(Marko 4:1-9; Luka 8:4-8)**

13 [d]Siku iyo hiyo Yesu akatoka nje
ya nyumba, akaketi kando ya
bahari. 2 [e]Umati mkubwa mno wa watu
ukakusanyika kumzunguka, hata ikabidi
aingie katika chombo na kuketi humo, nao
watu wote wakawa wamesimama ukingoni
mwa bahari. 3 [f]Ndipo akawaambia mambo
mengi kwa mifano, akisema: “Mpanzi
alitoka kwenda kupanda mbegu zake.
4 Alipokuwa akitawanya mbegu, nyingine
zilianguka kando ya njia, nao ndege wakaja
na kuzila. 5 Nyingine zilianguka kwenye
ardhi yenye mwamba isiyo na udongo wa
kutosha. Zikaota haraka, kwa kuwa udongo
ulikuwa haba. 6 Lakini jua lilipozidi, mimea
ikanyauka na kukauka kwa kuwa mizizi
yake haikuwa na kina. 7 Mbegu nyingine
zilianguka kwenye miiba, nayo miiba hiyo
ikakua, ikaisonga hiyo mimea. 8 [g]Mbegu
nyingine zilianguka kwenye udongo mzuri
ambapo zilitoa mazao, nyingine mara mia
moja, nyingine mara sitini, na nyingine
mara thelathini. 9 [h]Mwenye masikio ya
kusikia, na asikie.”

### *Sababu Ya Kufundisha Kwa Mifano*

**(Marko 4:10-12; Luka 8:9-10)**

10 Wanafunzi wake wakamwendea,
wakamuuliza, “Kwa nini unasema na watu
kwa mifano?”

11 [i]Akawajibu, “Ninyi mmepewa
kuzifahamu siri za Ufalme wa Mbinguni,
lakini wao hawajapewa. 12 [j]Kwa maana yule
aliye na kitu atapewa zaidi, naye atakuwa
navyo tele. Lakini yule asiye na kitu, hata
kile alicho nacho atanyang’anywa. 13 [k]Hii
ndiyo sababu nasema nao kwa mifano:

“Ingawa wanatazama, hawaoni;
wanasikiliza, lakini hawasikii,
wala hawaelewi.

14 [l]Kwao unatimia ule unabii wa Isaya
aliposema:

“ ‘Hakika mtasikiliza lakini
hamtaelewa;
na pia mtatazama lakini
hamtaona.
15 [m]Kwa kuwa mioyo ya watu hawa
imekuwa migumu;
hawasikii kwa masikio yao,
na wamefumba macho yao.
Wasije wakaona kwa macho yao,
na wakasikiliza kwa masikio yao,
wakaelewa kwa mioyo yao,
na kugeuka nami nikawaponya.’

16 [n]Lakini heri macho yenu kwa sababu
yanaona, na heri masikio yenu kwa sababu
yanasikia. 17 [o]Amin, nawaambia, manabii
wengi na wenye haki walitamani kuona
yale mnayoyaona lakini hawakuyaona,
na walitamani kusikia yale mnayoyasikia
lakini hawakuyasikia.

---

[a]**12:46** Lk 11:24; Ay 1:7; 1Pet 5:8
[b]**12:48** Lk 2:49
[c]**12:50** Mt 6:10; Yn 15:14
[d]**13:1** Mt 13:36; 9:28
[e]**13:2** Lk 5:3
[f]**13:3** Lk 8:5
[g]**13:8** Mwa 26:12
[h]**13:9** Mt 11:15
[i]**13:11** Kol 1:27; 1Yn 2:20, 27
[j]**13:12** Mt 25:29; Lk 19:26
[k]**13:13** Yer 5:21; Eze 12:2
[l]**13:14** Mt 1:22; 13:35; Eze 12:2; Isa 6:9; Mdo 28:26-28
[m]**13:15** Isa 6:9-10; Rum 11:8
[n]**13:16** Mt 16:17; Lk 10:23-24
[o]**13:17** Ebr 11:13; 1Pet 1:10-12

*Maelezo Ya Mfano Wa Mbegu*

**(Marko 4:13-20; Luka 8:11-15)**

[18] [a]“Sikilizeni basi maana ya ule mfano
wa mpanzi: [19] [b]Mtu yeyote anaposikia neno
la Ufalme naye asilielewe, yule mwovu huja
na kunyakua kile kilichopandwa moyoni
mwake. Hii ndiyo ile mbegu iliyopandwa
kando ya njia. [20] [c]Ile mbegu iliyopandwa
kwenye sehemu yenye mawe ni mtu yule
ambaye hulisikia neno na mara hulipokea
kwa furaha. [21] [d]Lakini kwa kuwa hana
mizizi yenye kina ndani yake, lile neno
hudumu kwa muda mfupi tu. Kisha dhiki
au mateso yanapoinuka kwa ajili ya lile
neno, yeye mara huchukizwa. [22] [e]Ile
mbegu iliyopandwa katika miiba ni yule
mtu alisikiaye neno, lakini masumbufu
ya maisha haya na udanganyifu wa mali
hulisonga lile neno na kulifanya lisizae
matunda. [23] [f]Lakini ile mbegu iliyopandwa
kwenye udongo mzuri ni yule mtu ambaye
hulisikia neno na kulielewa. Naye hakika
huzaa matunda, akizaa mara mia, au
mara sitini, au mara thelathini ya mbegu
iliyopandwa.”

*Mfano Wa Magugu*

[24] [g]Yesu akawaambia mfano mwingine,
akasema: “Ufalme wa Mbinguni unaweza
kufananishwa na mtu aliyepanda mbegu
nzuri katika shamba lake. [25] Lakini wakati
kila mtu alipokuwa amelala, adui yake
akaja na kupanda magugu katikati ya
ngano, akaenda zake. [26] Ngano ilipoota na
kutoa masuke, magugu nayo yakatokea.

[27] “Watumishi wa yule mwenye shamba
wakamjia na kumwambia, ‘Bwana, si
tulipanda mbegu nzuri shambani mwako?
Basi, magugu yametoka wapi?’

[28] “Akawajibu, ‘Adui ndiye alifanya
jambo hili.’

“Wale watumishi wakamuuliza, ‘Je,
unataka twende tukayang’oe?’

[29] “Lakini akasema, ‘Hapana, msiyang’oe,
kwa maana wakati mking’oa magugu
mnaweza mkang’oa na ngano pamoja nayo.
[30] [h]Acheni ngano na magugu vikue vyote
pamoja mpaka wakati wa mavuno. Wakati
huo nitawaambia wavunaji wayakusanye
magugu kwanza, wayafunge matita matita
ili yachomwe moto; kisha wakusanye ngano
na kuileta ghalani mwangu.’ ”

*Mfano Wa Mbegu Ya Haradali*

**(Marko 4:30-32; Luka 13:18-19)**

[31] [i]Akawaambia mfano mwingine,
akasema, “Ufalme wa Mbinguni ni kama
punje ya haradali, ambayo mtu aliichukua,
akaipanda shambani mwake. [32] [j]Ingawa
mbegu hiyo ni ndogo kuliko mbegu zote,
lakini inapokua ni mmea mkubwa kuliko
yote ya bustanini, nao huwa mti mkubwa,
hadi ndege wa angani wanakuja na
kutengeneza viota katika matawi yake.”

*Mfano Wa Chachu*

**(Luka 13:20-21)**

[33] [k]Akawaambia mfano mwingine,
“Ufalme wa Mbinguni unafanana na
chachu ambayo mwanamke aliichukua
akaichanganya katika kiasi kikubwa cha
unga mpaka wote ukaumuka.”

*Sababu Ya Yesu Kutumia Mifano*

**(Marko 4:33-34)**

[34] [l]Yesu alinena mambo haya yote kwa
makutano kwa mifano. Wala hakuwaambia
lolote pasipo mfano. [35] [m]Hii ilikuwa ili
kutimiza lile lililonenwa kwa kinywa cha
nabii aliposema:

> “Nitafungua kinywa changu niseme
> nao kwa mifano;
> nitahubiri mambo yaliyofichika
> tangu kuumbwa kwa misingi ya
> ulimwengu.”

---

[a]**13:18** Mk 4:14; Lk 8:11
[b]**13:19** Mt 4:23; 5:37
[c]**13:20** Isa 58:2; Eze 33:31, 32; Yn 5:35
[d]**13:21** Mt 11:6; 26:31
[e]**13:22** Mt 19:23; 1Tim 6:9-10, 17
[f]**13:23** Mt 13:8
[g]**13:24** Mt 25:1; Mk 4:26-39
[h]**13:30** Mt 3:12
[i]**13:31** Mt 17:20; Lk 17:6
[j]**13:32** Za 104:12; Dan 4:12
[k]**13:33** Mt 13:24; Mwa 18:6; Gal 5:9
[l]**13:34** Mk 4:33-34
[m]**13:35** Za 78:2; 1Kor 2:7

*Ufafanuzi Wa Mfano Wa Magugu*

36 [a]Kisha Yesu akaagana na makutano,
akaingia nyumbani. Wanafunzi wake
wakamjia wakamwambia, “Tueleze maana
ya ule mfano wa magugu shambani.”
37 [b]Akawaambia, “Aliyepanda mbegu
nzuri ni Mwana wa Adamu. 38 [c]Shamba ni
ulimwengu na mbegu nzuri ni wana wa
Ufalme. Magugu ni wana wa yule mwovu.
39 [d]Yule adui aliyepanda magugu ni ibilisi.
Mavuno ni mwisho wa dunia, nao wavunaji
ni malaika.
40 [e]“Kama vile magugu yang’olewavyo na
kuchomwa motoni, ndivyo itakavyokuwa
wakati wa mwisho wa dunia. 41 [f]Mwana
wa Adamu atawatuma malaika zake, nao
watakusanya kutoka Ufalme wake kila
kitu kinachosababisha dhambi na watenda
maovu wote. 42 [g]Nao watawatupa katika
tanuru la moto ambako kutakuwa na kilio
na kusaga meno. 43 [h]Ndipo wenye haki
watang’aa kama jua katika Ufalme wa Baba
yao. Yeye aliye na masikio, na asikie.

*Mfano Wa Hazina Iliyofichwa Na Lulu*

44 [i]“Ufalme wa Mbinguni unafanana
na hazina iliyofichwa shambani, ambayo
mtu mmoja alipoiona akaificha tena.
Kisha katika furaha yake, akaenda akauza
vyote alivyokuwa navyo, akalinunua lile
shamba.”
45 [j]“Tena, Ufalme wa Mbinguni unafanana
na mfanyabiashara aliyekuwa akitafuta lulu
safi. 46 [k]Alipoipata lulu moja ya thamani
kubwa, alikwenda akauza vyote alivyokuwa
navyo akainunua.”

*Mfano Wa Wavu*

47 [l]“Tena, Ufalme wa Mbinguni ni kama
wavu wa kuvua samaki uliotupwa baharini
ukavua samaki wa kila aina. 48 Ulipojaa,
wavuvi wakavuta pwani, wakaketi na
kukusanya samaki wazuri kuwaweka
kwenye vyombo safi, lakini wale samaki
wabaya wakawatupa. 49 [m]Hivi ndivyo
itakavyokuwa wakati wa mwisho wa dunia.
Malaika watakuja na kuwatenganisha
watu waovu na watu wenye haki. 50 [n]Nao
watawatupa hao waovu katika tanuru la
moto ambako kutakuwa na kilio na kusaga
meno.”
51 Yesu akauliza, “Je, mmeyaelewa haya
yote?”
Wakamjibu, “Ndiyo.”
52 [o]Akawaambia, “Basi kila mwalimu wa
sheria aliyefundishwa elimu ya Ufalme
wa Mbinguni ni kama mwenye nyumba
anayetoa kutoka ghala yake mali mpya na
mali ya zamani.”

*Yesu Akataliwa Nazareti*

**(Marko 6:1-6; Luka 4:16-30)**

53 [p]Yesu alipomaliza kutoa mifano hii,
akaondoka. 54 [q]Alipofika mji wa kwao,
akawafundisha watu katika sinagogi lao.
Nao wakastaajabu, wakauliza, “Mtu huyu
amepata wapi hekima hii na uwezo huu
wa kufanya miujiza?” 55 [r]“Huyu si yule
mwana wa seremala? Mama yake si yeye
aitwaye Maria, nao ndugu zake si Yakobo,
Yosefu, Simoni na Yuda? 56 [s]Nao dada zake
wote, hawako hapa pamoja nasi? Mtu huyu
amepata wapi basi mambo haya yote?”
57 [t]Wakachukizwa naye.
Lakini Yesu akawaambia, “Nabii hakosi
heshima, isipokuwa katika nchi yake na
nyumbani kwake.”
58 [u]Naye hakufanya miujiza mingi huko
kwa sababu ya kutokuamini kwao.

[a]**13:36** Mt 15:15; 13:24-30
[b]**13:37** Mt 8:20
[c]**13:38** Yn 8:44-45; 1Yn 3:10
[d]**13:39** Yoe 3:13; Mt 24:3; 28:20; Ufu 14:15
[e]**13:40** Yn 15:6
[f]**13:41** Mt 8:20; 24:31
[g]**13:42** Mt 13:50; 8:12
[h]**13:43** Dan 12:3; Mt 11:15
[i]**13:44** Mt 13:24; Isa 55:1; Flp 3:7-8
[j]**13:45** Mt 13:24
[k]**13:46** Mt 2:4; 3:14, 15; 8:10, 19
[l]**13:47** Mt 13:24; 22:9-10
[m]**13:49** Mt 25:32
[n]**13:50** Mt 8:12
[o]**13:52** Wim 7:13
[p]**13:53** Mt 7:28
[q]**13:54** Mt 4:23; 7:28
[r]**13:55** Lk 3:23; Yn 6:42; Mt 12:46
[s]**13:56** Yn 7:15, 52
[t]**13:57** Yn 6:61; Lk 4:24; Yn 4:44
[u]**13:58** Mk 6:5, 6

*Yohana Mbatizaji Akatwa Kichwa*

**(Marko 6:14-29; Luka 9:7-9)**

14 [a]Wakati huo, Mfalme Herode, mtawala
wa Galilaya, alisikia habari za Yesu,
2 [b]akawaambia watumishi wake, “Huyu ni
Yohana Mbatizaji; amefufuka kutoka kwa
wafu! Hii ndiyo sababu nguvu za kutenda
miujiza zinafanya kazi ndani yake.”

3 [c]Herode alikuwa amemkamata Yohana,
akamfunga na kumweka gerezani kwa
sababu ya Herodia, mke wa Filipo,
ndugu yake, 4 [d]kwa kuwa Yohana alikuwa
amemwambia Herode: “Si halali kwako
kuwa na huyo mwanamke.” 5 [e]Herode
alitaka sana kumuua Yohana, lakini
akaogopa watu, kwa maana walimtambua
kuwa ni nabii.

6 Katika siku ya kuadhimisha sikukuu ya
kuzaliwa kwa Herode, binti wa Herodia
alicheza mbele ya watu waliohudhuria,
akamfurahisha sana Herode, 7 kiasi kwamba
aliahidi kwa kiapo kumpa huyo binti
chochote angeomba. 8 Huyo binti, akiwa
amechochewa na mama yake, akasema,
“Nipe kichwa cha Yohana Mbatizaji
kwenye sinia.” 9 Mfalme akasikitika, lakini
kwa sababu ya viapo alivyoapa mbele ya
wageni, akaamuru kwamba apatiwe ombi
lake. 10 [f]Hivyo akaagiza Yohana Mbatizaji
akatwe kichwa mle gerezani. 11 Kichwa
chake kikaletwa kwenye sinia, akapewa
yule binti, naye akampelekea mama
yake. 12 [g]Wanafunzi wa Yohana wakaja na
kuuchukua mwili wake kwenda kuuzika.
Kisha wakaenda wakamwambia Yesu.

*Yesu Alisha Wanaume 5,000*

**(Marko 6:30-44; Luka 9:10-17; Yohana 6:1-14)**

13 [h]Yesu aliposikia yaliyokuwa yametukia,
aliondoka kwa chombo akaenda mahali
pasipo na watu ili awe peke yake. Lakini
watu walipopata habari, wakamfuata
kwa miguu kupitia nchi kavu kutoka
miji. 14 [i]Yesu alipofika kando ya bahari,
aliona makutano makubwa ya watu,
akawahurumia na akawaponya wagonjwa
wao.

15 [j]Ilipofika jioni, wanafunzi wake
walienda kwake, wakamwambia, “Mahali
hapa ni nyikani, na muda sasa umekwisha.
Waage makutano ili waende zao vijijini
wakajinunulie chakula.”

16 Yesu akawaambia, “Hakuna sababu
ya wao kuondoka. Ninyi wapeni chakula.”

17 [k]Wakamjibu, “Tuna mikate mitano na
samaki wawili tu.”

18 Akawaambia, “Nileteeni hivyo vitu
hapa.” 19 [l]Yesu akaagiza makutano wakae
chini kwenye nyasi. Akaichukua ile
mikate mitano na wale samaki wawili,
akainua macho yake akatazama mbinguni,
akavibariki na kuimega ile mikate. Kisha
akawapa wanafunzi, nao wanafunzi
wakawagawia makutano. 20 [m]Wote wakala,
wakashiba. Nao wanafunzi wakakusanya
vipande vilivyosalia, wakajaza vikapu
kumi na viwili. 21 Idadi ya watu waliokula
walikuwa wanaume wapatao 5,000, bila
kuhesabu wanawake na watoto.

*Yesu Atembea Juu Ya Maji*

**(Marko 6:45-52; Yohana 6:15-21)**

22 [n]Mara Yesu akawaambia wanafunzi
wake waingie kwenye mashua watangulie
kwenda ng’ambo ya bahari, wakati yeye
alikuwa akiwaaga wale makutano. 23 [o]Baada
ya kuwaaga, akaenda zake mlimani
peke yake kuomba. Jioni ilipofika, Yesu
alikuwa huko peke yake. 24 Wakati huo ile
mashua ilikuwa mbali kutoka nchi kavu
ikisukwasukwa na mawimbi, kwa sababu
upepo ulikuwa wa mbisho.

---

[a]**14:1** Lk 13:31; 9:7-9; Mdo 12:1
[b]**14:2** Mt 3:1
[c]**14:3** Mt 4:12; 11:2; Lk 3:19-20
[d]**14:4** Law 18:16; 20:21
[e]**14:5** Mt 11:19; 21:26; Lk 20:26
[f]**14:10** Mt 17:12
[g]**14:12** Mt 8:2
[h]**14:13** Mk 6:31-44; Mt 10:23; Mk 6:32; Lk 9:19; Yn 6:13
[i]**14:14** Mt 9:36; 4:23
[j]**14:15** Mk 6:35; Lk 9:12; Yn 6:5
[k]**14:17** Mt 16:9; 1Sam 9:13; 1Kor 10:16
[l]**14:19** Mt 15:36; 1Sam 9:13; Mt 26:26; Mk 8:6; Lk 9:16; 24:30; Mdo 2:42; 20:7
[m]**14:20** 2Fal 4:44
[n]**14:22** Mk 6:45-46
[o]**14:23** Lk 3:21; 6:12; 9:18

25 Wakati wa zamu ya nne ya usiku,[a]
Yesu akawaendea wanafunzi wake akiwa
anatembea juu ya maji. 26 [b]Wanafunzi wake
walipomwona akitembea juu ya maji,
waliingiwa na hofu kuu, wakasema, “Ni
mzimu.” Wakapiga yowe kwa kuogopa.
27 [c]Lakini mara Yesu akasema nao,
akawaambia, “Jipeni moyo! Ni mimi.
Msiogope.”
28 Petro akamjibu, “Bwana, ikiwa ni
wewe, niambie nije kwako nikitembea juu
ya maji.”
29 Yesu akamwambia, “Njoo.”
Basi Petro akatoka kwenye chombo,
akatembea juu ya maji kumwelekea Yesu.
30 Lakini alipoona upepo mkali aliingiwa na
hofu, naye akaanza kuzama, huku akipiga
kelele, “Bwana, niokoe!”
31 [d]Mara Yesu akaunyoosha mkono
wake na kumshika, akamwambia, “Wewe
mwenye imani haba, kwa nini uliona
shaka?”
32 Nao walipoingia ndani ya mashua,
upepo ukakoma. 33 [e]Ndipo wote waliokuwa
ndani ya ile mashua wakamwabudu Yesu,
wakisema, “Hakika, wewe ndiwe Mwana
wa Mungu.”

### *Yesu Awaponya Wagonjwa Genesareti*

**(Marko 6:53-56)**

34 Walipokwisha kuvuka, wakafika
nchi ya Genesareti. 35 Watu wa eneo lile
walipomtambua Yesu, walipeleka habari
sehemu zote za jirani. Watu wakamletea
wagonjwa wao wote, 36 [f]wakamsihi
awaruhusu wagonjwa waguse tu pindo
la vazi lake, nao wote waliomgusa,
wakaponywa.

### *Mapokeo Ya Wazee*

**(Marko 7:1-13)**

15 [g]Ndipo baadhi ya Mafarisayo na walimu
wa sheria wakamjia Yesu kutoka
Yerusalemu na kumuuliza, 2 [h]“Mbona
wanafunzi wako wanakiuka mapokeo ya
wazee? Kwa maana wao hawanawi mikono
yao kabla ya kula!”
3 Yesu akawajibu, “Mbona ninyi
mnavunja amri ya Mungu kwa ajili ya
mapokeo yenu? 4 [i]Kwa maana Mungu
alisema, ‘Waheshimu baba yako na mama
yako,’ na, ‘Yeyote amtukanaye baba yake
au mama yake, na auawe.’ 5 [j]Lakini ninyi
mwafundisha kwamba mtu akimwambia
baba yake au mama yake, ‘Kile ambacho
ningeweza kukusaidia kimewekwa wakfu
kwa Mungu,’ 6 basi hana tena sababu ya
kumheshimu baba yake nacho. Basi kwa
ajili ya mafundisho yenu mnavunja amri
ya Mungu. 7 [k]Ninyi wanafiki! Isaya alikuwa
sawa alipotabiri juu yenu kwamba:

8 [l]“ ‘Watu hawa huniheshimu kwa
midomo yao,
lakini mioyo yao iko mbali nami.
9 [m]Huniabudu bure;
nayo mafundisho yao
ni maagizo ya wanadamu tu.’ ”

### *Vitu Vitiavyo Unajisi*

**(Marko 7:14-23)**

10 [n]Yesu akaita ule umati wa watu,
akawaambia, “Sikilizeni na mwelewe:
11 [o]kinachomfanya mtu kuwa najisi mbele za
Mungu si kile kiingiacho kinywani mwake,
bali ni kile kitokacho kinywani mwake.”
12 Kisha wanafunzi wake wakamjia na
kumuuliza, “Je, unajua kwamba Mafarisayo
walichukizwa sana waliposikia yale
uliyosema?”

---

[a]25 Zamu ya nne ya usiku ni kati ya saa tisa na saa kumi na mbili asubuhi.
[b]**14:26** Lk 24:37; Ay 9:8
[c]**14:27** Mt 9:2; Mdo 23:11; Dan 10:12; Mdo 18:9
[d]**14:31** Mt 6:30
[e]**14:33** Za 2:7; Mt 4:3
[f]**14:36** Mt 9:20-21
[g]**15:1** Mk 7:1-23
[h]**15:2** Kum 4:2; Lk 11:38; Kum 4:2; Lk 11:38
[i]**15:4** Kut 20:12; Efe 6:2; Kut 21:17; Law 9:20; Kut 20:12; Efe 6:2; Kut 21:17; Law 9:20
[j]**15:5** Mk 7:11, 12
[k]**15:7** Isa 29:13
[l]**15:8** Isa 29:11; Eze 33:31
[m]**15:9** Kol 2:20-22; Isa 29:13; Mal 2:2
[n]**15:10** Mk 7:14
[o]**15:11** Mdo 10:14-15

13 [a]Akawajibu, “Kila pando ambalo
Baba yangu wa mbinguni hakulipanda,
litang’olewa. 14 [b]Waacheni; wao ni viongozi
vipofu, wanaoongoza vipofu. Kama kipofu
akimwongoza kipofu mwenzake, wote
wawili watatumbukia shimoni.”
15 [c]Petro akasema, “Tueleze maana ya
huu mfano.”
16 [d]Yesu akawauliza, “Je, bado ninyi
hamfahamu? 17 [e]Je, hamwelewi kwamba
chochote kiingiacho kinywani huenda
tumboni, na hatimaye hutolewa nje kikiwa
uchafu? 18 [f]Lakini kitokacho kinywani
hutoka moyoni, na hiki ndicho kimtiacho
mtu unajisi. 19 [g]Kwa maana ndani ya moyo
hutoka mawazo mabaya, uuaji, uzinzi,
uasherati, wizi, ushahidi wa uongo na
masingizio. 20 [h]Haya ndiyo yamtiayo mtu
unajisi; lakini kula bila kunawa mikono
hakumtii mtu unajisi.”

*Imani Ya Mwanamke Mkanaani*

**(Marko 7:24-30)**

21 [i]Yesu aliondoka mahali pale, akaenda
sehemu za Tiro na Sidoni. 22 [j]Mwanamke
mmoja Mkanaani aliyeishi sehemu jirani
na hizo akaja kwake akilia, akasema,
“Nihurumie, Ee Bwana, Mwana wa Daudi!
Binti yangu amepagawa na pepo mchafu,
na anateseka sana.”
23 Lakini Yesu hakumjibu neno. Hivyo
wanafunzi wake wakamwendea na kumsihi
sana, wakisema, “Mwambie aende zake,
kwa maana anaendelea kutupigia kelele.”
24 [k]Yesu akajibu, “Nimetumwa tu kwa
ajili ya kondoo wa Israeli waliopotea.”
25 [l]Lakini yule mwanamke akaja, akapiga
magoti mbele ya Yesu, akasema, “Bwana,
nisaidie!”
26 Yesu akajibu, “Si haki kuchukua
chakula cha watoto na kuwatupia mbwa.”
27 Yule mwanamke akajibu, “Ndiyo,
Bwana, lakini hata mbwa hula makombo
yanayoanguka kutoka kwenye meza za
bwana zao.”
28 [m]Ndipo Yesu akamwambia,
“Mwanamke, imani yako ni kubwa! Iwe
kwako kama unavyotaka.” Naye binti yake
akapona tangu saa ile.

*Yesu Aponya Watu Wengi*

29 Yesu akaondoka na kwenda kando
ya Bahari ya Galilaya. Kisha akapanda
mlimani, akaketi huko. 30 [n]Umati mkubwa
wa watu ukamjia, wakiwaleta vilema,
vipofu, viwete, bubu na wengine wengi,
wakawaweka miguuni pake; naye
akawaponya. 31 [o]Hao watu wakashangaa
walipoona bubu wakisema, vilema
wakipona, viwete wakitembea na vipofu
wakiona, wakamtukuza Mungu wa Israeli.

*Yesu Alisha Watu Elfu Nne*

**(Marko 8:1-10)**

32 [p]Kisha Yesu akawaita wanafunzi wake,
akawaambia, “Ninauhurumia huu umati wa
watu, kwa sababu sasa wamekuwa pamoja
nami kwa muda wa siku tatu, na hawana
chakula chochote. Nami sipendi kuwaaga
wakiwa na njaa, wasije wakazimia njiani.”
33 Wanafunzi wake wakasema, “Tutapata
wapi mikate ya kutosha kuwalisha umati
huu wa watu mkubwa namna hii, nasi tuko
nyikani?”
34 Yesu akawauliza, “Mnayo mikate
mingapi?”
Wakamjibu, “Tunayo mikate saba na
visamaki vichache.”
35 Yesu akawaambia ule umati wa watu
waketi chini. 36 [q]Kisha akachukua ile
mikate saba na wale samaki, naye akiisha
kumshukuru Mungu, akavimega na kuwapa

[a]**15:13** Isa 60:21; Yn 15:2
[b]**15:14** Mt 23:16, 24; Rum 2:19; Lk 6:9
[c]**15:15** Mt 13:36
[d]**15:16** Mt 16:9
[e]**15:17** 1Nya 6:13
[f]**15:18** Lk 6:45; Yak 3:6
[g]**15:19** Gal 5:19-21
[h]**15:20** Rum 14:14
[i]**15:21** Mt 11:21
[j]**15:22** Mt 9:27; 4:24
[k]**15:24** Mt 10:6, 23; Rum 15:8
[l]**15:25** Mt 8:2; Yn 12:25; Lk 17:33
[m]**15:28** Mt 9:22
[n]**15:30** Mt 4:23
[o]**15:31** Mt 9:8
[p]**15:32** Mt 14:19
[q]**15:36** Mt 14:19

wanafunzi wake, nao wakawapa ule umati
wa watu. 37 [a]Wote wakala na kushiba.
Baadaye wanafunzi wakakusanya vipande
vilivyosalia, wakajaza vikapu saba. 38 Idadi
ya watu walikuwa wanaume 4,000, bila
kuhesabu wanawake na watoto. 39 Baada
ya kuaga ule umati wa watu, Yesu aliingia
katika mashua, akaenda sehemu za
Magadani.[b]

*Mafarisayo Wadai Ishara*

**(Marko 8:11-13; Luka 12:54-56)**

16 [c]Mafarisayo na Masadukayo wakamjia
Yesu na kumjaribu kwa kumwomba
awaonyeshe ishara kutoka mbinguni.
2 [d]Yesu akawajibu, "Ifikapo jioni,
mnasema, 'Hali ya hewa itakuwa nzuri, kwa
kuwa anga ni nyekundu.' 3 [e]Nanyi wakati
wa asubuhi mnasema, 'Leo kutakuwa na
dhoruba, kwa sababu anga ni nyekundu
na mawingu yametanda.' Mnajua jinsi
ya kupambanua kule kuonekana kwa
anga, lakini hamwezi kupambanua dalili
za nyakati. 4 [f]Kizazi kiovu na cha uzinzi
kinatafuta ishara, lakini hakitapewa ishara
yoyote isipokuwa ishara ya Yona." Yesu
akawaacha, akaenda zake.

*Chachu Ya Mafarisayo Na Masadukayo*

**(Marko 8:14-21)**

5 [g]Wanafunzi wake walipofika ng'ambo
ya bahari, walikuwa wamesahau kuchukua
mikate. 6 [h]Yesu akawaambia, "Jihadharini.
Jilindeni na chachu ya Mafarisayo na ya
Masadukayo."
7 Wakajadiliana wao kwa wao, wakisema,
"Ni kwa sababu hatukuleta mikate."
8 [i]Yesu, akifahamu majadiliano
yao, akauliza, "Enyi wa imani haba!
Mbona mnajadiliana miongoni mwenu
kuhusu kutokuwa na mikate? 9 [j]Je, bado
hamwelewi? Je, hamkumbuki ile mikate
mitano iliyolisha watu 5,000 na idadi ya
vikapu vingapi vya mabaki mlivyokusanya?
10 [k]Au ile mikate saba iliyolisha watu 4,000
na idadi ya vikapu vingapi vya mabaki
mlivyokusanya? 11 Inakuwaje mnashindwa
kuelewa kwamba nilikuwa sisemi nanyi
habari za mikate? Jilindeni na chachu ya
Mafarisayo na Masadukayo." 12 [l]Ndipo
wakaelewa kwamba alikuwa hasemi juu ya
chachu ya kutengeneza mikate, bali juu ya
mafundisho ya Mafarisayo na Masadukayo.

*Petro Amkiri Yesu Kuwa Ni Mwana Wa Mungu*

**(Marko 8:27-30; Luka 9:18-21)**

13 [m]Basi Yesu alipofika katika eneo la
Kaisaria-Filipi, akawauliza wanafunzi wake,
"Watu husema kwamba mimi Mwana wa
Adamu ni nani?"
14 [n]Wakamjibu, "Baadhi husema ni
Yohana Mbatizaji; wengine husema ni
Eliya; na bado wengine husema ni Yeremia
au mmojawapo wa manabii."
15 Akawauliza, "Je, ninyi mnasema mimi
ni nani?"
16 [o]Simoni Petro akamjibu, "Wewe ndiwe
Kristo,[p] Mwana wa Mungu aliye hai."
17 [q]Naye Yesu akamwambia, "Heri
wewe, Simoni Bar-Yona,[r] kwa maana hili
halikufunuliwa kwako na mwanadamu, bali
na Baba yangu aliye mbinguni. 18 [s]Nami
nakuambia, wewe ndiwe Petro na juu ya
mwamba huu nitalijenga kanisa langu,
hata malango ya Kuzimu hayataweza
kulishinda. 19 [t]Nitakupa funguo za Ufalme

[a]**15:37** Mt 16:10
[b]39 Magadani ni Magdala, mji wa Galilaya, kama kilomita 16 kusini mwa Kapernaumu.
[c]**16:1** Mdo 4:1; Mt 12:38
[d]**16:2** Lk 12:54-56
[e]**16:3** Lk 12:54-56
[f]**16:4** Mt 12:39
[g]**16:5** Mk 8:14
[h]**16:6** Lk 12:1
[i]**16:8** Mt 6:30
[j]**16:9** Mt 14:17-21
[k]**16:10** Mt 15:34-38
[l]**16:12** Yn 6:27; Mdo 4:1
[m]**16:13** Mk 8:27; Lk 9:18
[n]**16:14** Mt 3:1; 14:2; Mk 6:15; Yn 1:21; Mt 14:2; Lk 9:7, 8, 9
[o]**16:16** Yer 10:10; Yn 11:27
[p]16 *Kristo* maana yake ni *Masiya*, yaani *Aliyetiwa mafuta.*
[q]**16:17** Gal 1:16; Efe 6:12
[r]17 Bar-Yona ni neno la Kiaramu, maana yake ni Mwana wa Yona.
[s]**16:18** Yn 1:42; Efe 2:20
[t]**16:19** Isa 22:22; Ufu 3:7; Mt 18:18; Yn 20:23

wa mbinguni, na lolote utakalolifunga duniani litakuwa limefungwa Mbinguni, nalo lolote utakalofungua duniani litakuwa limefunguliwa mbinguni.” [20] [a] Kisha akawakataza wanafunzi wake wasimwambie mtu yeyote kwamba yeye ndiye Kristo.

*Yesu Anatabiri Juu Ya Kifo Chake*

**(Marko 8:31–9:1; Luka 9:22-27)**

[21] [b]Tangu wakati huo, Yesu alianza kuwaeleza wanafunzi wake kwamba hana budi kwenda Yerusalemu na kupata mateso mengi mikononi mwa wazee, viongozi wa makuhani, na walimu wa sheria, na kwamba itampasa auawe lakini siku ya tatu kufufuliwa.

[22] Petro akamchukua kando, akaanza kumkemea akisema, “Haiwezekani, Bwana! Jambo hili kamwe halitakupata!”

[23] [c]Lakini Yesu akageuka na kumwambia Petro, “Rudi nyuma yangu, Shetani! Wewe ni kikwazo kwangu. Moyo wako hauwazi yaliyo ya Mungu, bali ya wanadamu.”

[24] [d]Ndipo Yesu akawaambia wanafunzi wake, “Mtu yeyote akitaka kunifuata, ni lazima ajikane mwenyewe, auchukue msalaba wake, anifuate. [25] [e]Kwa maana yeyote anayetaka kuyaokoa maisha yake atayapoteza, lakini yeyote atakayeyapoteza maisha yake kwa ajili yangu atayapata. [26] [f]Kwa maana, je, itamfaidi nini mtu kuupata ulimwengu wote, lakini akayapoteza maisha yake? Au mtu atatoa nini badala ya nafsi yake? [27] [g]Kwa maana Mwana wa Adamu atakuja katika utukufu wa Baba yake pamoja na malaika zake, naye ndipo atakapomlipa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake. [28] [h]Nawaambia kweli, baadhi yenu hapa hawataonja mauti kabla ya kumwona Mwana wa Adamu akija katika Ufalme wake.”

*Yesu Abadilika Sura Mlimani*

**(Marko 9:2-13; Luka 9:28-36)**

17 [i]Siku sita baada ya jambo hili, Yesu akawachukua Petro, Yakobo na Yohana ndugu yake Yakobo, akawapeleka juu ya mlima mrefu peke yao. [2] [j]Wakiwa huko, Yesu alibadilika sura mbele yao. Uso wake ukang’aa kama jua na nguo zake zikawa na weupe wa kuumiza macho. [3] Ghafula wakawatokea mbele yao Mose na Eliya, wakizungumza na Yesu.

[4] Ndipo Petro akamwambia Yesu, “Bwana, ni vyema sisi tukae hapa. Ukitaka, nitafanya vibanda vitatu: kimoja chako, kingine cha Mose na kingine cha Eliya.”

[5] [k]Petro alipokuwa angali ananena, ghafula wingu lililong’aa likawafunika, na sauti ikatoka kwenye hilo wingu ikisema, “Huyu ni Mwanangu mpendwa. Ninapendezwa naye sana. Msikieni yeye.”

[6] [l]Wanafunzi waliposikia haya, wakaanguka chini kifudifudi, wakajawa na hofu. [7] [m]Lakini Yesu akaja na kuwagusa, akawaambia, “Inukeni na wala msiogope.” [8] Walipoinua macho yao, hawakumwona mtu mwingine yeyote isipokuwa Yesu.

[9] [n]Walipokuwa wakishuka kutoka mlimani, Yesu akawaagiza, “Msimwambie mtu yeyote mambo mliyoyaona hapa, mpaka Mwana wa Adamu atakapofufuliwa kutoka kwa wafu.”

[10] [o]Wale wanafunzi wakamuuliza, “Kwa nini basi walimu wa sheria husema kwamba ni lazima Eliya aje kwanza?”

[11] [p]Yesu akawajibu, “Ni kweli, Eliya lazima aje kwanza, naye atatengeneza mambo yote. [12] [q]Lakini nawaambia, Eliya

[a] **16:20** Mt 8:30
[b] **16:21** Za 22:6; Yn 19:3; Hos 6:2; 1Kor 15:3-4; Lk 18:31-33; 9:22
[c] **16:23** Mt 4:10
[d] **16:24** Mt 10:38-39; Lk 14:27
[e] **16:25** Yn 12:25
[f] **16:26** Za 49; Mt 4:8
[g] **16:27** Mt 8:20; 1Kor 1:7; Ufu 22:7; 2Nya 6:23; 2Kor 5:10
[h] **16:28** Mk 9:1; Lk 9:27; Mt 10:23
[i] **17:1** Mk 9:2; Lk 9:28; Mt 4:21
[j] **17:2** 2Pet 1:16-18
[k] **17:5** Mt 3:17; 2Pet 1:17; Mdo 3:22-23
[l] **17:6** 2Pet 1:18
[m] **17:7** Mt 14:27
[n] **17:9** Mk 8:30; Mt 8:20; 16:21; Mk 8:30; Mt 8:20; 16:21
[o] **17:10** Mt 11:14; Mal 4:5
[p] **17:11** Mal 4:5-6; Lk 1:16-17
[q] **17:12** Mt 11:14; 14:3, 10; 16:21

amekwisha kuja, nao hawakumtambua, bali
walimtendea kila kitu walichotaka. Vivyo
hivyo Mwana wa Adamu pia atateswa
mikononi mwao." 13 [a]Ndipo wale wanafunzi
wakaelewa kuwa alikuwa anazungumza
nao habari za Yohana Mbatizaji.

*Yesu Amponya Kijana Mwenye Pepo*

**(Marko 9:14-29; Luka 9:37-43)**

14 [b]Walipofika penye umati wa watu,
mtu mmoja akamjia Yesu na kupiga
magoti mbele yake, akasema, 15 [c]"Bwana,
mhurumie mwanangu. Yeye ana kifafa na
anateseka sana. Mara kwa mara huanguka
kwenye moto au kwenye maji. 16 Nilimleta
kwa wanafunzi wako, lakini hawakuweza
kumponya."

17 [d]Yesu akajibu, "Enyi kizazi kisichoamini
na kilichopotoka! Nitakaa nanyi mpaka
lini? Nitawavumilia mpaka lini? Mleteni
mvulana hapa kwangu." 18 Yesu akamkemea
yule pepo mchafu, akamtoka yule kijana,
naye akapona saa ile ile.

19 [e]Kisha wanafunzi wakamwendea Yesu
wakiwa peke yao, wakamuuliza, "Kwa nini
sisi hatukuweza kumtoa?"

20 [f]Akawajibu, "Kwa sababu ya imani
yenu ndogo. Ninawaambia kweli, mkiwa
na imani ndogo kama punje ya haradali,
mtauambia mlima huu, 'Ondoka hapa uende
pale,' nao utaondoka. Wala hakutakuwa na
jambo lisilowezekana kwenu. [ 21 Lakini
hali kama hii haitoki ila kwa kuomba na
kufunga.]"

22 [g]Siku moja walipokuwa pamoja huko
Galilaya, Yesu akawaambia, "Mwana wa
Adamu atasalitiwa na kutiwa mikononi
mwa watu. 23 [h]Nao watamuua, lakini siku ya
tatu atafufuliwa." Wanafunzi wakahuzunika
sana.

*Yesu Na Petro Watoa Kodi Ya Hekalu*

24 [i]Baada ya Yesu na wanafunzi wake
kufika Kapernaumu, wakusanya kodi ya
Hekalu[j] wakamjia Petro na kumuuliza, "Je,
Mwalimu wenu halipi kodi ya Hekalu?"

25 [k]Petro akajibu, "Ndiyo, yeye hulipa."
Petro aliporudi nyumbani, Yesu akawa
wa kwanza kulizungumzia, akamuuliza,
"Unaonaje Simoni? Wafalme wa dunia
hupokea ushuru na kodi kutoka kwa nani?
Je, ni kutoka kwa watoto wao au kutoka
kwa watu wengine?"

26 Petro akamjibu, "Kutoka kwa watu
wengine." Yesu akamwambia, "Kwa hiyo
watoto wao wamesamehewa. 27 [l]Lakini ili
tusije tukawaudhi, nenda baharini ukatupe
ndoana. Mchukue samaki wa kwanza
utakayemvua. Fungua kinywa chake nawe
utakuta humo fedha, ichukue ukalipe kodi
yako na yangu."

*Aliye Mkuu Katika Ufalme Wa Mbinguni*

**(Marko 9:33-37; Luka 9:46-48)**

18 [m]Wakati huo, wanafunzi wakamjia
Yesu na kumuuliza, "Je, nani aliye
mkuu kuliko wote katika Ufalme wa
Mbinguni?"

2 Yesu akamwita mtoto mdogo na
kumsimamisha katikati yao. 3 [n]Naye
akasema: "Amin, nawaambia, msipookoka
na kuwa kama watoto wadogo, kamwe
hamtaingia katika Ufalme wa Mbinguni.
4 [o]Kwa hiyo mtu yeyote anyenyekeaye kama
huyu mtoto, ndiye aliye mkuu kuliko wote
katika Ufalme wa Mbinguni.

5 [p]"Yeyote amkaribishaye mtoto mdogo
kama huyu kwa Jina langu, anikaribisha
mimi. 6 [q]Lakini kama mtu yeyote
akimsababisha mmojawapo wa hawa

---

[a]**17:13** Lk 1:17
[b]**17:14** Mk 9:14-20
[c]**17:15** Mt 4:24
[d]**17:17** Kum 32:5; Yn 14:9
[e]**17:19** Mt 10:1
[f]**17:20** Mt 21:21; Mk 11:23; Lk 17:6; 1Kor 13:2
[g]**17:22** Mt 8:20
[h]**17:23** Mdo 2:23; 3:13; Mt 16:21
[i]**17:24** Kut 30:13
[j]24 Kodi ya Hekalu ilikuwa didrachmas, yaani drakma mbili, ambazo ni sawa na nusu shekeli.
[k]**17:25** Mt 12:17-21; Rum 13:7
[l]**17:27** Yn 6:61
[m]**18:1** Mk 9:33; Lk 9:46; 22:24
[n]**18:3** Mt 19:14; 2Pet 2:2; Mt 3:2
[o]**18:4** Mk 9:35
[p]**18:5** Mt 10:40; Yn 13:20
[q]**18:6** Mt 5:29; Mk 9:42; Lk 17:2

wadogo wanaoniamini kutenda dhambi,
ingekuwa bora kwake afungiwe jiwe kubwa
la kusagia shingoni mwake, na kutoswa
katika kilindi cha bahari.

### *Kujaribiwa Ili Kutenda Dhambi*

**(Marko 9:42-48; Luka 17:1-2)**

7 [a]“Ole kwa ulimwengu kwa sababu ya
yale mambo yanayosababisha watu kutenda
dhambi! Mambo hayo lazima yawepo, lakini
ole wake mtu yule ambaye huyasababisha.
8 [b]Ikiwa mkono wako au mguu wako
unakusababisha utende dhambi, ukate na
uutupe mbali. Ni afadhali kwako kuingia
katika uzima ukiwa huna mkono mmoja
au mguu mmoja, kuliko kuwa na mikono
miwili au miguu miwili, na kutupwa
katika moto wa milele. 9 [c]Nalo jicho lako
likikusababisha kutenda dhambi, ling’oe,
ulitupe mbali. Ni afadhali kwako kuingia
katika uzima ukiwa na jicho moja, kuliko
kuwa na macho mawili lakini ukatupwa
katika moto wa jehanamu.

### *Mfano Wa Kondoo Aliyepotea*

**(Luka 15:3-7)**

10 [d]“Angalia ili usimdharau mmojawapo
wa hawa wadogo, kwa maana nawaambia,
malaika wao mbinguni daima wanauona
uso wa Baba yangu aliye mbinguni. [
11 [e]Kwa maana Mwana wa Adamu alikuja
kuokoa kile kilichopotea.]
12 [f]“Mwaonaje? Ikiwa mtu ana kondoo
mia moja, na mmoja wao akapotea, je,
hatawaacha wale tisini na tisa vilimani na
kwenda kumtafuta huyo mmoja aliyepotea?
13 [g]Naye akishampata, amin, nawaambia,
hufurahi zaidi kwa ajili ya huyo kondoo
mmoja kuliko wale tisini na tisa ambao
hawakupotea. 14 Vivyo hivyo, Baba yenu
wa mbinguni hapendi hata mmojawapo wa
hawa wadogo apotee.

### *Ndugu Yako Akikukosea*

15 [h]“Kama ndugu yako akikukosea, nenda
ukamwonyeshe kosa lake, kati yenu ninyi
wawili peke yenu. Kama akikusikiliza,
utakuwa umempata tena ndugu yako.
16 [i]Lakini kama hatakusikiliza, nenda
na mtu mwingine mmoja au wawili ili
kila neno lithibitishwe kwa ushahidi wa
mashahidi wawili au watatu. 17 [j]Kama
akikataa kuwasikiliza hao, liambie kanisa.
Naye kama akikataa hata kulisikiliza kanisa,
basi awe kwenu kama mtu asiyeamini au
mtoza ushuru.
18 [k]“Amin, nawaambia, lolote
mtakalolifunga duniani litakuwa
limefungwa mbinguni, na lolote
mtakalolifungua duniani litakuwa
limefunguliwa mbinguni.
19 [l]“Tena nawaambia, ikiwa wawili wenu
watakubaliana duniani kuhusu jambo
lolote watakaloomba, watafanyiwa na
Baba yangu aliye mbinguni. 20 [m]Kwa kuwa
wanapokusanyika pamoja watu wawili au
watatu kwa Jina langu, mimi niko papo
hapo pamoja nao.”

### *Kusamehe*

21 [n]Ndipo Petro akamjia Yesu na
kumuuliza, “Bwana, ndugu yangu anikosee
mara ngapi nami nimsamehe? Je, hata mara
saba?”
22 [o]Yesu akamjibu, “Sikuambii hata mara
saba, bali hata saba mara sabini.

### *Mfano Wa Mtumishi Asiyesamehe*

23 [p]“Kwa hiyo Ufalme wa Mbinguni
unaweza kufananishwa na mfalme aliyetaka
kufanya hesabu zake za fedha na watumishi
wake. 24 Alipoanza kufanya hesabu zake,
mtu mmoja aliyekuwa anadaiwa talanta[q]

[a]**18:7** Lk 17:1
[b]**18:8** Mt 5:28; Mk 9:43-45
[c]**18:9** Mt 5:22, 29
[d]**18:10** Za 34:7; Ebr 1:14
[e]**18:11** Lk 9:36; 19:10; Yn 1:17; 12:47
[f]**18:12** Lk 15:4
[g]**18:13** Lk 1:17
[h]**18:15** Law 19:17; Gal 6:1
[i]**18:16** Kum 17:6; Ebr 10:28
[j]**18:17** 1Kor 6:1-6; Rum 16:17; 2The 3:6, 14
[k]**18:18** Mt 16:18; Yn 20:23
[l]**18:19** Mt 7:7
[m]**18:20** Mt 28:20; Yn 14:23
[n]**18:21** Mt 6:14; Lk 17:4
[o]**18:22** Mwa 4:24
[p]**18:23** Mt 13:24; 25:19
[q]24 Talanta moja ni sawa na mshahara wa kibarua wa miaka 15.

10,000, aliletwa kwake. 25 [a]Kwa kuwa
alikuwa hawezi kulipa deni hilo, bwana
wake akaamuru kwamba auzwe, yeye,
mkewe, watoto wake na vyote alivyokuwa
navyo, ili lile deni lipate kulipwa.

26 [b]“Yule mtumishi akampigia magoti,
akamsihi yule bwana akisema, ‘Naomba
univumilie, nami nitakulipa deni lako
lote.’ 27 Yule bwana wa huyo mtumishi
akamwonea huruma, akafuta deni lake lote,
akamwacha aende zake.

28 “Lakini yule mtumishi alipokuwa
anatoka nje, akakutana na mtumishi
mwenzake aliyekuwa amemkopesha dinari[c]
mia moja. Akamkamata, akamkaba koo
akimwambia, ‘Nilipe kile ninachokudai!’

29 “Yule mtumishi mwenzake akapiga
magoti akamsihi akisema, ‘Naomba
univumilie, nami nitakulipa deni lako lote.’

30 “Lakini akakataa. Badala yake, alienda
akamtupa gerezani hata atakapolipa hilo
deni. 31 Watumishi wenzake walipoona
haya yaliyotukia wakaudhika sana, nao
wakaenda na kumwambia bwana wao kila
kitu kilichokuwa kimetukia.

32 “Yule bwana akamwita yule mtumishi
akamwambia, ‘Wewe mtumishi mwovu!
Mimi nilikusamehe deni lako lote uliponisihi.
33 Je, haikukupasa kumhurumia mtumishi
mwenzako kama mimi nilivyokuhurumia
wewe?’ 34 [d]Kwa hasira, yule bwana
wake akamtia yule mtumishi mikononi
mwa askari wa gereza ili ateswe mpaka
atakapolipa yote aliyokuwa anadaiwa.

35 [e]“Hivi ndivyo Baba yangu wa mbinguni
atakavyomfanyia kila mmoja wenu ikiwa
hatamsamehe ndugu yake kutoka moyoni
mwake.”

### *Yesu Afundisha Kuhusu Talaka*

**(Marko 10:1-12)**

19 [f]Yesu alipomaliza kusema maneno
haya, aliondoka Galilaya, akaenda
sehemu za Uyahudi, ng’ambo ya Mto
Yordani. 2 [g]Umati mkubwa wa watu
ukamfuata, naye akawaponya huko.

3 [h]Baadhi ya Mafarisayo wakamjia ili
kumjaribu, wakamuuliza, “Ni halali mtu
kumwacha mke wake kwa sababu yoyote?”

4 [i]Akawajibu, “Je, hamkusoma kwamba
hapo mwanzo Muumba aliwaumba
mwanaume na mwanamke, 5 [j]naye
akasema, ‘Kwa sababu hii mwanaume
atamwacha baba yake na mama yake,
naye ataambatana na mkewe, na hao
wawili watakuwa mwili mmoja’? 6 [k]Hivyo
si wawili tena, bali mwili mmoja. Kwa hiyo
alichokiunganisha Mungu, mwanadamu
asikitenganishe.”

7 [l]Wakamuuliza, “Kwa nini basi Mose
aliagiza mtu kumpa mkewe hati ya talaka
na kumwacha?”

8 Yesu akawajibu, “Mose aliwaruhusu
kuwaacha wake zenu kwa sababu ya ugumu
wa mioyo yenu. Lakini tangu mwanzo
haikuwa hivyo. 9 [m]Mimi nawaambia, yeyote
amwachaye mkewe isipokuwa kwa sababu
ya uasherati naye akaoa mke mwingine,
anazini. Naye amwoaye yule mwanamke
aliyeachwa pia anazini.”

10 [n]Wanafunzi wake wakamwambia,
“Kama hali ndiyo hii kati ya mume na mke,
ni afadhali mtu asioe!”

11 [o]Yesu akawaambia, “Si watu wote
wanaoweza kupokea neno hili, isipokuwa
wale tu waliojaliwa na Mungu. 12 [p]Kwa
maana wengine ni matowashi kwa sababu
wamezaliwa hivyo; wengine wamefanywa
matowashi na wanadamu; na wengine
wamejifanya matowashi kwa ajili ya Ufalme
wa Mbinguni. Yeye awezaye kulipokea
neno hili na alipokee.”

---

[a]**18:25** Lk 7:42; 2Fal 4:1; Neh 5:5-8
[b]**18:26** Mt 8:2
[c]28 Dinari moja ilikuwa kama mshahara wa kibarua wa siku moja.
[d]**18:34** Mt 5:26
[e]**18:35** Mt 6:14; Yak 2:13
[f]**19:1** Mt 7:28
[g]**19:2** Mt 4:23
[h]**19:3** Mt 5:31
[i]**19:4** Mwa 1:27; 5:2
[j]**19:5** Mwa 2:24; Efe 5:31
[k]**19:6** 1Kor 7:10, 11
[l]**19:7** Kum 24:1-4; Mt 5:31-32
[m]**19:9** Lk 16:18
[n]**19:10** Mit 21:19
[o]**19:11** Mit 13:11; 1Kor 7:7-9, 17
[p]**19:12** 1Kor 7:12, 14; 9:5, 15

*Yesu Awabariki Watoto Wadogo*

**(Marko 10:13-16; Luka 18:15-17)**

13 [a]Kisha watoto wadogo wakaletwa
kwa Yesu ili aweke mikono yake juu yao
na awaombee. Lakini wanafunzi wake
wakawakemea wale waliowaleta.
14 [b]Yesu akasema, “Waacheni watoto
wadogo waje kwangu, wala msiwazuie,
kwa maana Ufalme wa Mbinguni ni wa
wale walio kama hawa.” 15 Naye akaweka
mikono yake juu yao, na akaondoka huko.

*Kijana Tajiri*

**(Marko 10:17-31; Luka 18:18-30)**

16 [c]Mtu mmoja akamjia Yesu na
kumuuliza, “Mwalimu mwema, nifanye
jambo gani jema ili nipate uzima wa
milele?”
17 [d]Yesu akamjibu, “Mbona unaniuliza
habari ya mema? Aliye mwema ni Mmoja
tu. Lakini ukitaka kuingia uzimani, zitii
amri.”
18 [e]Yule mtu akamuuliza, “Amri zipi?”
Yesu akamjibu, “Usiue, usizini, usiibe,
usishuhudie uongo, 19 [f]waheshimu baba
yako na mama yako, na umpende jirani
yako kama nafsi yako.”
20 Yule kijana akasema, “Hizi zote
nimezishika. Je, bado nimepungukiwa na
nini?”
21 [g]Yesu akamwambia, “Kama ukitaka
kuwa mkamilifu, nenda, ukauze vitu vyote
ulivyo navyo, na hizo fedha uwape maskini,
nawe utakuwa na hazina mbinguni. Kisha
njoo, unifuate.”
22 [h]Yule kijana aliposikia hayo, akaenda
zake kwa huzuni, kwa sababu alikuwa na
mali nyingi.

*Hatari Za Utajiri*

23 [i]Ndipo Yesu akawaambia wanafunzi
wake, “Amin, nawaambia, itakuwa vigumu
kwa mtu tajiri kuingia katika Ufalme wa
Mbinguni. 24 Tena nawaambia, ni rahisi
zaidi kwa ngamia kupita kwenye tundu la
sindano kuliko mtu tajiri kuingia katika
Ufalme wa Mungu.”
25 Wanafunzi wake waliposikia haya,
walishangaa sana na kuuliza, “Ni nani basi
awezaye kuokoka?”
26 [j]Lakini Yesu akawatazama,
akawaambia, “Kwa mwanadamu jambo
hili haliwezekani, lakini mambo yote
yanawezekana kwa Mungu.”
27 [k]Ndipo Petro akamjibu, “Tazama, sisi
tumeacha kila kitu na kukufuata! Tutapata
nini basi?”
28 [l]Yesu akawaambia, “Amin, nawaambia,
wakati wa kufanywa upya vitu vyote,
Mwana wa Adamu atakapoketi kwenye kiti
chake kitukufu cha enzi, ninyi mlionifuata
pia mtaketi katika viti vya enzi kumi na
viwili, mkiyahukumu makabila kumi na
mawili ya Israeli. 29 [m]Kila mtu aliyeacha
nyumba, au ndugu zake wa kiume au wa
kike, baba au mama, watoto au mashamba
kwa ajili yangu, atapokea mara mia zaidi
ya hayo, naataurithi uzima wa milele.
30 [n]Lakini wengi walio wa kwanza watakuwa
wa mwisho, na walio wa mwisho watakuwa
wa kwanza.

*Mfano Wa Wafanyakazi Katika Shamba La Mizabibu*

20 [o]“Kwa maana Ufalme wa Mbinguni
unafanana na mtu mwenye shamba
aliyetoka alfajiri ili kwenda kuajiri
vibarua kufanya kazi katika shamba lake
la mizabibu. 2 Baada ya kukubaliana na hao

---

[a]**19:13** Mk 5:23
[b]**19:14** Mt 23:34; 18:3; 1Pet 2:2
[c]**19:16** Mt 25:46; Lk 10:25
[d]**19:17** Law 18:5
[e]**19:18** Yak 2:11
[f]**19:19** Kut 20:12-16; Kum 5:16-20; Law 19:18; Mt 5:43
[g]**19:21** Mt 5:48; Lk 12:33; Mdo 4:34-35; Mt 6:20
[h]**19:22** Za 62:10
[i]**19:23** Mt 13:22; 1Tim 6:9-10
[j]**19:26** Zek 8:6; Rum 4:21; Lk 18:28; Kum 33:9; Mt 4:20; Lk 5:11
[k]**19:27** Mt 4:19
[l]**19:28** Mt 20:21; 25:31; Lk 22:28-30; Ufu 3:21; Lk 22:28, 29, 30; 1Kor 6:2, 3; Ufu 2:26
[m]**19:29** Mt 6:33; 25:46; Mk 10:29, 30; Lk 18:29, 30
[n]**19:30** Mk 10:33; Lk 10:30
[o]**20:1** Mt 13:24; 21:28, 33

vibarua kuwalipa ujira wa dinari[a] moja kwa
siku, akawapeleka kwenye shamba lake la
mizabibu.
3 “Mnamo saa tatu akatoka tena,
akawakuta wengine wamesimama sokoni
bila kazi. 4 Akawaambia, ‘Ninyi nanyi
nendeni mkafanye kazi katika shamba langu
la mizabibu, nami nitawalipa chochote
kilicho haki yenu.’ 5 Kwa hiyo wakaenda.
“Akatoka tena mnamo saa sita na pia
saa tisa akafanya vivyo hivyo. 6 Mnamo
saa kumi na moja akatoka tena akawakuta
wengine bado wamesimama bila kazi.
Akawauliza, ‘Kwa nini mmesimama hapa
kutwa nzima pasipo kufanya kazi?’
7 “Wakamjibu, ‘Ni kwa sababu hakuna
yeyote aliyetuajiri.’
“Akawaambia, ‘Ninyi nanyi nendeni
mkafanye kazi katika shamba langu la
mizabibu.’
8 [b]“Ilipofika jioni, yule mwenye shamba
la mizabibu akamwambia msimamizi,
‘Waite hao vibarua na uwalipe ujira wao,
ukianzia na wale walioajiriwa mwisho na
kuishia na wale walioajiriwa kwanza.’
9 “Wale vibarua walioajiriwa mnamo
saa kumi na moja, wakaja na kila mmoja
wao akapokea dinari moja. 10 Hivyo wale
walioajiriwa kwanza walipofika, walidhani
watalipwa zaidi. Lakini kila mmoja wao
pia alipokea dinari moja. 11 [c]Walipoipokea,
wakaanza kulalamika dhidi ya yule
mwenye shamba, 12 [d]wakisema, ‘Hawa watu
walioajiriwa mwisho wamefanya kazi kwa
muda wa saa moja tu, nawe umewafanya
sawa na sisi ambao tumestahimili taabu na
joto lote la mchana kutwa?’
13 [e]“Yule mwenye shamba akamjibu
mmoja wao, ‘Rafiki, sijakudhulumu. Je,
hukukubaliana nami kwa ujira wa kawaida
wa dinari moja? 14 Chukua ujira wako na
uende. Mimi nimeamua kumlipa huyu mtu
aliyeajiriwa mwisho kama nilivyokupa
wewe. 15 [f]Je, sina haki yangu kufanya
kile nitakacho na mali yangu mwenyewe?
Au unaona wivu kwa kuwa nimekuwa
mkarimu?’
16 [g]“Vivyo hivyo, wa mwisho watakuwa
wa kwanza, na wa kwanza watakuwa wa
mwisho.”

*Yesu Atabiri Tena Kuhusu Kifo Chake*

**(Marko 10:32-34; Luka 18:31-34)**

17 [h]Basi Yesu alipokuwa anapanda
kwenda Yerusalemu, aliwachukua kando
wale wanafunzi wake kumi na wawili
na kuwaambia, 18 [i]“Tunapanda kwenda
Yerusalemu, na Mwana wa Adamu atatiwa
mikononi mwa viongozi wa makuhani na
walimu wa sheria. Nao watamhukumu
kifo 19 [j]na kumtia mikononi mwa watu
wa Mataifa ili wamdhihaki na kumpiga
mijeledi na kumsulubisha msalabani. Naye
atafufuliwa siku ya tatu!”

*Ombi La Mama Yake Yakobo Na Yohana*

**(Marko 10:35-45)**

20 [k]Kisha mama yao wana wa Zebedayo
akamjia Yesu pamoja na wanawe, naye
akapiga magoti mbele yake, akamwomba
Yesu amfanyie jambo fulani.
21 [l]Yesu akamuuliza, “Unataka nini?”
Akajibu, “Tafadhali, wajalie wanangu hawa
ili mmoja aketi upande wako wa kuume, na
mwingine upande wako wa kushoto katika
Ufalme wako.”
22 [m]Yesu akawaambia, “Ninyi hamjui
mnaloliomba. Je, mnaweza kukinywea
kikombe nitakachonywea mimi?”
Wakajibu, “Tunaweza.”
23 [n]Yesu akawaambia, “Kwa kweli
kikombe changu mtakinywea, lakini kuketi
upande wangu wa kuume au wa kushoto si

---

[a]2 Dinari moja ilikuwa kama mshahara wa kibarua wa siku moja.
[b]**20:8** Law 19:13; Kum 24:15
[c]**20:11** Yn 4:1
[d]**20:12** Yn 4:8; Yak 1:11
[e]**20:13** Mt 22:12; 26:50
[f]**20:15** Kum 15:9; Mk 7:22
[g]**20:16** Mt 19:30
[h]**20:17** Mk 10:32; Lk 18:31; Yn 12:12
[i]**20:18** Lk 9:51; Mt 8:20; 16:21; 27:1-2
[j]**20:19** Mdo 2:23; Mt 16:21
[k]**20:20** Mt 4:21; 8:2
[l]**20:21** Mt 19:28
[m]**20:22** Yer 49:12; Yn 18:11
[n]**20:23** Mdo 12:2; Ufu 1:9

langu mimi kuwapa. Nafasi hizo ni za wale
ambao wameandaliwa na Baba yangu."
24 [a]Wale wanafunzi wengine kumi
waliposikia haya, waliwakasirikia hao
ndugu wawili. 25 Lakini Yesu akawaita
wote pamoja na kuwaambia, "Mnafahamu
kuwa watawala wa watu wa Mataifa
huwatawala kwa nguvu, nao wenye vyeo
huonyesha mamlaka yao. 26 [b]Isiwe hivyo
kwenu. Badala yake, yeyote anayetaka
kuwa mkuu miongoni mwenu hana budi
kuwa mtumishi wenu, 27 [c]naye anayetaka
kuwa wa kwanza miongoni mwenu hana
budi kuwa mtumwa wenu: 28 [d]kama vile
ambavyo Mwana wa Adamu hakuja ili
kutumikiwa, bali kutumika na kuutoa uhai
wake uwe fidia kwa ajili ya wengi."

### *Yesu Awaponya Vipofu Wawili*

**(Marko 10:46-52; Luka 18:35-43)**

29 [e]Yesu na wanafunzi wake walipokuwa
wakiondoka Yeriko, umati mkubwa wa
watu ulimfuata. 30 [f]Vipofu wawili walikuwa
wameketi kando ya barabara. Waliposikia
kwamba Yesu alikuwa anapita, wakapiga
kelele wakisema, "Bwana, Mwana wa
Daudi, tuhurumie!"
31 Ule umati wa watu ukawakemea
na kuwaambia wanyamaze, lakini wao
wakazidi kupaza sauti, wakisema, "Bwana,
Mwana wa Daudi, tuhurumie."
32 Yesu akasimama na kuwaita,
akawauliza, "Mnataka niwafanyie nini?"
33 Wakamjibu, "Bwana, tunataka kuona."
34 Yesu akawahurumia na kuwagusa
macho yao. Mara macho yao yakapata
kuona, nao wakamfuata.

### *Yesu Anaingia Yerusalemu Kwa Shangwe*

**(Marko 11:1-11; Luka 19:28-40; Yohana 12:12-19)**

21 [g]Walipokaribia Yerusalemu, wakafika
Bethfage katika Mlima wa Mizeituni.
Ndipo Yesu akawatuma wanafunzi wake
wawili, 2 akawaambia, "Nendeni katika
kijiji kilichoko mbele yenu, nanyi mtamkuta
punda amefungwa hapo, na mwana-punda
pamoja naye. Wafungueni na mniletee.
3 [h]Kama mtu yeyote akiwasemesha lolote,
mwambieni kwamba Bwana ana haja nao,
naye atawaruhusu mwalete mara."
4 [i]Haya yalitukia ili litimie lile lililonenwa
na nabii, akisema:

5 [j]"Mwambieni Binti Sayuni,
'Tazama, mfalme wako anakuja
kwako,
ni mnyenyekevu, naye amepanda
punda,
juu ya mwana-punda, mtoto wa
punda.' "

6 [k]Wale wanafunzi wakaenda, wakafanya
kama Yesu alivyokuwa amewaagiza.
7 [l]Wakamleta yule punda na mwana-
punda, nao wakatandika mavazi yao juu
ya hao punda, naye Yesu akaketi juu yake.
8 [m]Umati mkubwa wa watu ukatandaza
mavazi yao barabarani, na wengine
wakakata matawi kutoka kwenye miti,
wakayatandaza barabarani. 9 [n]Ule umati
wa watu uliomtangulia na ule uliomfuata
ukapiga kelele ukisema,

---

[a]**20:24** Lk 22:24-25
[b]**20:26** Mt 22:11; Mk 9:35
[c]**20:27** Mt 18:4; Mk 9:35
[d]**20:28** Mt 8:20; Isa 42:1; Flp 2:8; Kut 30:2; Ebr 9:28
[e]**20:29** Mk 10:46; Lk 18:35
[f]**20:30** Mt 9:27; 15:22
[g]**21:1** Yn 8:1; Mdo 1:12
[h]**21:3** Mt 26:18
[i]**21:4** Mt 1:22
[j]**21:5** Zek 9:9; Isa 62:11
[k]**21:6** Mk 11:4
[l]**21:7** 1Fal 9:13
[m]**21:8** 2Fal 9:3
[n]**21:9** Mt 9:27; Za 118:26; Mt 23:29; Lk 2:14

"Hosana,[a] Mwana wa Daudi!"

"Amebarikiwa yeye ajaye kwa Jina
la Bwana!"

"Hosana juu mbinguni!"

10 [b]Yesu alipoingia Yerusalemu, mji wote
ukataharuki, watu wakauliza, "Huyu ni
nani?"
11 [c]Ule umati wa watu ukajibu, "Huyu
ni Yesu, yule nabii kutoka Nazareti katika
Galilaya."

*Yesu Atakasa Hekalu*

**(Marko 11:15-19; Luka 19:45-48; Yohana 2:13-22)**

12 [d]Yesu akaingia katika eneo la Hekalu
na kuwafukuza wote waliokuwa wakinunua
na kuuza vitu Hekaluni. Akazipindua meza
za wale waliokuwa wakibadilisha fedha, na
pia viti vya wale waliokuwa wakiuza njiwa.
13 [e]Akawaambia, "Imeandikwa, 'Nyumba
yangu itaitwa nyumba ya sala,' lakini ninyi
mmeifanya kuwa pango la wanyang'anyi."
14 [f]Vipofu na vilema wakamwendea kule
Hekaluni, naye akawaponya. 15 [g]Lakini
viongozi wa makuhani na walimu wa sheria
walipoona mambo ya ajabu aliyofanya na
kuwasikia watoto wakishangilia katika eneo
la Hekalu wakisema, "Hosana Mwana wa
Daudi," walikasirika.
16 [h]Wakamuuliza Yesu, "Je, unasikia hayo
hawa wanayosema?"

Akawajibu, "Naam; kwani hamkusoma,

" 'Midomoni mwa watoto wachanga
na wanyonyao
umeamuru sifa'?"

17 [i]Akawaacha, akatoka nje ya mji,
akaenda hadi Bethania, akalala huko.

*Mtini Wanyauka*

**(Marko 11:12-14, 20-24)**

18 [j]Asubuhi na mapema, Yesu alipokuwa
akirudi mjini, alikuwa na njaa. 19 [k]Akauona
mtini kando ya barabara, naye akaukaribia,
lakini hakupata tunda lolote ila majani.
Ndipo akauambia, "Wewe usizae matunda
tena kamwe!" Papo hapo ule mtini
ukanyauka.
20 [l]Wanafunzi wake walipoona jambo hili,
wakashangaa, wakamuuliza, "Imekuwaje
mtini huu kunyauka ghafula?"
21 [m]Yesu akawajibu, "Amin, nawaambia,
kama mkiwa na imani wala msiwe na
shaka, si kwamba mtaweza kufanya tu
yale yaliyofanyika kwa huu mtini, bali
hata mkiuambia huu mlima, 'Ng'oka,
ukatupwe baharini,' litafanyika. 22 [n]Yoyote
mtakayoyaomba mkisali na mkiamini,
mtayapokea."

*Wahoji Kuhusu Mamlaka Ya Yesu*

**(Marko 11:27-33; Luka 20:1-8)**

23 [o]Yesu alipoingia Hekaluni, viongozi
wa makuhani na wazee wa watu wakamjia
alipokuwa anafundisha na kusema,
"Unafanya mambo haya kwa mamlaka
gani? Na ni nani aliyekupa mamlaka hayo?"
24 Yesu akawajibu, "Nami nitawauliza
swali moja. Kama mkinijibu, nami
nitawaambia ni kwa mamlaka gani
ninafanya mambo haya. 25 Ubatizo wa
Yohana, ulitoka wapi? Je, ulitoka mbinguni
au kwa wanadamu?"

Wakahojiana wao kwa wao na kusema,
"Tukisema ulitoka mbinguni atatuuliza,
'Mbona basi hamkumwamini?' 26 [p]Lakini
tukisema, 'Ulitoka kwa wanadamu,'
tunawaogopa hawa watu, maana wote
wanamtambua Yohana kuwa ni nabii."
27 Kwa hiyo wakamjibu Yesu, "Sisi
hatujui."

Naye akawaambia, "Wala mimi

[a]9 Kiebrania kusema Okoa, basi likawa neno la shangwe.
[b]**21:10** Mk 11:15; Lk 19:45; Yn 2:13, 15
[c]**21:11** Kum 18:15; Yn 1:21
[d]**21:12** Kum 14:26; Kut 30:13; Law 1:14
[e]**21:13** Isa 56:7; Yer 7:11
[f]**21:14** Mt 4:23
[g]**21:15** Mt 9:27; Lk 19:39
[h]**21:16** Za 8:2
[i]**21:17** Lk 24:50; Yn 11:18
[j]**21:18** Mk 11:12
[k]**21:19** Isa 34:4; Yer 8:13
[l]**21:20** Mk 11:20
[m]**21:21** 1Kor 13:2; Yak 1:6
[n]**21:22** Mt 7:7
[o]**21:23** Mdo 4:7; 7:27
[p]**21:26** Mt 11:9; Mk 6:20

sitawaambia ni kwa mamlaka gani
ninatenda mambo haya.”

*Mfano Wa Wana Wawili*

28 [a]“Lakini mwaonaje? Mtu mmoja
alikuwa na wana wawili. Akamwendea
yule wa kwanza akamwambia, ‘Mwanangu,
nenda ukafanye kazi kwenye shamba la
mizabibu leo.’
29 [b]“Yule mwanawe akamjibu ‘Mimi
sitakwenda.’ Baadaye akabadili mawazo
yake akaenda.
30 “Kisha yule baba akamwendea yule
mwanawe mwingine akamwambia vilevile.
Yeye akajibu, ‘Nitakwenda, bwana,’ lakini
hakwenda.
31 [c]“Ni yupi kati yao hao wawili aliyetimiza
kile alichotaka baba yake?”
Wakamjibu, “Ni yule wa kwanza.”
Yesu akawaambia, “Amin, amin
nawaambia, watoza ushuru na makahaba
wanawatangulia kuingia katika Ufalme
wa Mungu. 32 [d]Kwa maana Yohana alikuja
kwenu kuwaonyesha njia ya haki, lakini
hamkumsadiki, lakini watoza ushuru
na makahaba wakamsadiki. Nanyi hata
mlipoona hayo, baadaye hamkutubu na
kumsadiki.

*Mfano Wa Wapangaji Waovu*

**(Marko 12:1-12; Luka 20:9-19)**

33 [e]“Sikilizeni mfano mwingine: Kulikuwa
na mtu mmoja mwenye shamba ambaye
alipanda shamba la mizabibu. Akajenga
ukuta kulizunguka, akatengeneza shinikizo
ndani yake na akajenga mnara wa ulinzi.
Kisha akalikodisha hilo shamba la mizabibu
kwa wakulima fulani, naye akaondoka,
akasafiri kwenda nchi nyingine. 34 [f]Wakati
wa mavuno ulipokaribia, akawatuma
watumishi wake kwa hao wapangaji ili
kukusanya matunda yake.
35 [g]“Wale wapangaji wakawakamata
wale watumishi, wakampiga mmoja,
wakamuua mwingine, na yule wa tatu
wakampiga mawe. 36 [h]Kisha akawatuma
kwao watumishi wengine, wengi kuliko
wale wa kwanza, nao wale wapangaji
wakawatendea vilevile. 37 Mwisho wa
yote, akamtuma mwanawe kwao, akisema,
‘Watamheshimu mwanangu.’
38 [i]“Lakini wale wapangaji walipomwona
mwanawe, wakasemezana wao kwa wao,
‘Huyu ndiye mrithi. Njooni tumuue,
ili tuchukue urithi wake.’ 39 [j]Hivyo
wakamchukua, wakamtupa nje ya shamba
la mizabibu, wakamuua.
40 “Kwa hiyo, huyo mwenye shamba la
mizabibu atakapokuja, atawafanyia nini
hao wakulima?”
41 [k]Wakamjibu, “Kwa huzuni kuu
atawaangamiza kabisa hao wadhalimu
na kulipangisha shamba lake la mizabibu
kwa wakulima wengine ambao watampatia
fungu lake la matunda wakati wa mavuno.”
42 [l]Yesu akawaambia, “Je, hamjasoma
katika Maandiko kwamba:

“ ‘Jiwe walilolikataa waashi
limekuwa jiwe kuu la pembeni.
Bwana ndiye alitenda jambo hili,
nalo ni la ajabu machoni petu’?

43 [m]“Kwa hiyo ninawaambia, Ufalme wa
Mungu utaondolewa kwenu na kupewa
watu wengine wawezao kuzaa matunda
yake. 44 [n]Yeye aangukaye juu ya jiwe hili
atavunjika vipande vipande, lakini yule
litakayemwangukia atasagwa kabisa.”
45 Viongozi wa Makuhani na Mafarisayo
waliposikia mifano ya Yesu, walitambua
kuwa alikuwa akiwasema wao.
46 [o]Wakatafuta njia ya kumkamata, lakini

---

[a]**21:28** Mt 21:33; 20:1
[b]**21:29** Mt 7:21
[c]**21:31** Lk 7:29; 7:50
[d]**21:32** Mt 3:1-12; Lk 3:12-13; 7:29-30; 7:36-50
[e]**21:33** Za 80:8; Isa 5:1-7; Mt 25:14-25
[f]**21:34** Mt 22:3
[g]**21:35** 2Nya 24:1; Ebr 11:36-37
[h]**21:36** Mt 22:4
[i]**21:38** Ebr 1:2; Mt 12:14; Za 2:8
[j]**21:39** Mt 26:50; Mk 14:46; Lk 22:54; Yn 18:12; Mdo 2:32
[k]**21:41** Mt 8:11-12; Mdo 18:6; 28:28
[l]**21:42** Za 118:22-23; 1Pet 2:7
[m]**21:43** Mt 8:12
[n]**21:44** Lk 2:34
[o]**21:46** Mt 21:11, 26

wakaogopa umati wa watu, kwa kuwa watu
walimwona Yesu kuwa ni nabii.

### *Mfano Wa Karamu Ya Arusi*

**(Luka 14:15-24)**

22 [a]Yesu akasema nao tena kwa mifano,
akawaambia, 2 [b]"Ufalme wa Mbinguni
unaweza kufananishwa na mfalme mmoja
aliyemwandalia mwanawe karamu ya arusi.
3 [c]Akawatuma watumishi wake kuwaita
wale waliokuwa wamealikwa karamuni,
lakini wakakataa kuja.
4 [d]"Kisha akawatuma watumishi wengine
akisema, 'Waambieni wale walioalikwa
kwamba nimeandaa chakula. Nimekwisha
kuchinja mafahali wangu na vinono,
karamu iko tayari. Karibuni kwa karamu
ya arusi.'
5 "Lakini hawakuzingatia, wakaenda
zao: huyu shambani mwake na mwingine
kwenye biashara zake. 6 Wengine wao
wakawakamata wale watumishi wake,
wakawatesa na kuwaua. 7 [e]Yule mfalme
akakasirika sana, akapeleka jeshi lake
likawaangamiza wale wauaji na kuuteketeza
mji wao kwa moto.
8 [f]"Kisha akawaambia watumishi wake,
'Karamu ya arusi imeshakuwa tayari,
lakini wale niliowaalika hawakustahili
kuja. 9 [g]Kwa hiyo nendeni katika njia
panda mkamwalike karamuni yeyote
mtakayemwona.' 10 [h]Wale watumishi
wakaenda barabarani, wakawakusanya
watu wote waliowaona, wema na wabaya.
Ukumbi wa arusi ukajaa wageni.
11 [i]"Lakini mfalme alipoingia ndani ili
kuwaona wageni, akamwona mle mtu
mmoja ambaye hakuwa amevaa vazi la
arusi. 12 [j]Mfalme akamuuliza, 'Rafiki,
uliingiaje humu bila vazi la arusi?' Yule
mtu hakuwa na la kusema.
13 [k]"Ndipo mfalme akawaambia
watumishi wake, 'Mfungeni mikono na
miguu mkamtupe nje, kwenye giza. Huko
kutakuwa na kilio na kusaga meno.'
14 [l]"Kwa maana walioitwa ni wengi, lakini
walioteuliwa ni wachache."

### *Kulipa Kodi Kwa Kaisari*

**(Marko 12:13-17; Luka 20:20-26)**

15 [m]Ndipo Mafarisayo wakatoka nje
wakaandaa mpango wa kumtega Yesu katika
maneno yake. 16 [n]Wakatuma wanafunzi
wao kwake pamoja na Maherode. Nao
wakasema, "Mwalimu, tunajua kwamba
wewe ni mtu mwadilifu na unafundisha njia
ya Mungu katika kweli bila kuyumbishwa na
mtu wala kuonyesha upendeleo. 17 [o]Tuambie
basi, wewe unaonaje? Je, ni halali kulipa
kodi kwa Kaisari, au la?"
18 Lakini Yesu, akijua makusudi yao
mabaya, akawaambia, "Enyi wanafiki, kwa
nini mnajaribu kunitega? 19 Nionyesheni
hiyo sarafu inayotumika kwa kulipia kodi."
Wakamletea dinari. 20 Naye akawauliza,
"Sura hii ni ya nani? Na maandishi haya
ni ya nani?"
21 [p]Wakamjibu, "Ni vya Kaisari."
Basi Yesu akawaambia, "Mpeni Kaisari
kilicho cha Kaisari, naye Mungu mpeni
kilicho cha Mungu."
22 [q]Waliposikia hili, wakashangaa. Hivyo
wakamwacha, wakaenda zao.

### *Ndoa Na Ufufuo*

**(Marko 12:18-27; Luka 20:27-40)**

23 [r]Siku hiyo hiyo Masadukayo, wale
wasemao kwamba hakuna ufufuo wa
wafu, wakamjia Yesu na kumuuliza swali,
wakisema, 24 [s]"Mwalimu, Mose alisema,

[a]**22:1** Lk 14:16; Ufu 19:7-9
[b]**22:2** Mt 13:24; Yn 3:29
[c]**22:3** Mt 21:34
[d]**22:4** Mt 21:36
[e]**22:7** Lk 19:27
[f]**22:8** Mt 10:11-13
[g]**22:9** Eze 21:21; Mt 13:47; 21:43
[h]**22:10** Mt 13:47-48
[i]**22:11** 2Kor 5:3; Efe 4:24; Kol 3:10, 12; Ufu 3:4; 16:15; 19:8
[j]**22:12** Mt 20:12; 26:50
[k]**22:13** Mt 8:12
[l]**22:14** Ufu 17:14; Mt 20:16
[m]**22:15** Mk 12:13; Lk 20:20
[n]**22:16** Mk 3:6
[o]**22:17** Mt 17:25
[p]**22:21** Rum 13:7
[q]**22:22** Mk 12:12
[r]**22:23** Mdo 4:1; 23:8; 1Kor 15:12
[s]**22:24** Kum 25:5-6

'Kama mtu akifa bila kuwa na watoto,
ndugu yake inampasa amwoe huyo
mjane ili ampatie watoto huyo nduguye
aliyekufa.' 25 Basi palikuwa na ndugu saba
miongoni mwetu. Yule wa kwanza akaoa
mke, naye akafa, na kwa kuwa hakuwa
na watoto, akamwachia nduguye yule
mjane. 26 Ikatokea vivyo hivyo kwa yule
ndugu wa pili, na wa tatu, hadi wote saba.
27 Hatimaye, yule mwanamke naye akafa.
28 Sasa basi, siku ya ufufuo, yeye atakuwa
mke wa nani miongoni mwa wale ndugu
saba, kwa kuwa wote walikuwa wamemwoa
huyo mwanamke?"
29 [a]Yesu akawajibu, "Mwapotoka kwa
sababu hamjui Maandiko wala uweza
wa Mungu. 30 [b]Wakati wa ufufuo, watu
hawataoa wala kuolewa, bali watakuwa
kama malaika wa mbinguni. 31 Lakini
kuhusu ufufuo wa wafu, hamjasoma kile
Mungu alichowaambia, kwamba, 32 [c]'Mimi
ni Mungu wa Abrahamu, Mungu wa Isaki,
na Mungu wa Yakobo'? Yeye si Mungu wa
wafu, bali ni Mungu wa walio hai."
33 [d]Ule umati wa watu uliposikia hayo,
ulishangaa sana kwa mafundisho yake.

### *Amri Kuu Kuliko Zote*

**(Marko 12:28-34; Luka 10:25-28)**

34 [e]Mafarisayo waliposikia kwamba Yesu
alikuwa amewanyamazisha Masadukayo,
Mafarisayo wakakusanyika pamoja.
35 [f]Mmoja wao, mtaalamu wa sheria,
akamuuliza swali ili kumjaribu, akisema,
36 "Mwalimu, ni amri ipi katika Sheria iliyo
kuu kuliko zote?"
37 [g]Yesu akamjibu, " 'Mpende Bwana
Mungu wako kwa moyo wako wote na
kwa roho yako yote na kwa akili zako
zote.' 38 Hii ndiyo amri iliyo kuu, tena ni
ya kwanza. 39 [h]Nayo ya pili ni kama hiyo,
nayo ni hii: 'Mpende jirani yako kama nafsi
yako.' 40 [i]Amri hizi mbili ndizo msingi wa
Sheria na Manabii."

### *Swali Kuhusu Mwana Wa Daudi*

**(Marko 12:35-37; Luka 20:41-44)**

41 [j]Wakati Mafarisayo walikuwa
wamekusanyika pamoja, Yesu akawauliza,
42 [k]"Mnaonaje kuhusu Kristo?[l] Yeye ni
mwana wa nani?"
Wakamjibu, "Yeye ni mwana wa Daudi."
43 Akawaambia, "Inakuwaje basi kwamba
Daudi, akinena kwa kuongozwa na Roho,
anamwita Kristo 'Bwana'? Kwa maana
asema,

44 [m]" 'Bwana alimwambia Bwana
wangu:
"Keti mkono wangu wa kuume,
hadi nitakapowaweka adui zako
chini ya miguu yako." '

45 Kama basi Daudi anamwita yeye 'Bwana,'
awezaje kuwa mwanawe?" 46 [n]Hakuna mtu
aliyeweza kumjibu Yesu neno. Tena tangu
siku hiyo hakuna aliyethubutu kumuuliza
tena maswali.

### *Yesu Awashutumu Walimu Wa Sheria Na Mafarisayo*

**(Marko 12:38-40; Luka 11:39-52; 20:45-47)**

23 [o]Kisha Yesu akauambia umati wa
watu pamoja na wanafunzi wake:
2 [p]"Walimu wa sheria na Mafarisayo
wameketi katika kiti cha Mose, 3 [q]hivyo
inawapasa kuwatii na kufanya kila kitu
wanachowaambia. Lakini msifuate yale
wanayotenda, kwa sababu hawatendi
yale wanayohubiri. 4 [r]Wao hufunga mizigo
mikubwa na kuiweka mabegani mwa watu,

---

[a]**22:29** Yn 20:9
[b]**22:30** Mt 24:38
[c]**22:32** Kut 3:6; Mdo 7:32
[d]**22:33** Mt 7:28
[e]**22:34** Mdo 4:1
[f]**22:35** Lk 11:45; 14:3
[g]**22:37** Kum 6:5
[h]**22:39** Law 19:18; Gal 5:14
[i]**22:40** Mt 7:12; Lk 10:25-28
[j]**22:41** Mk 12:35; Lk 20:41
[k]**22:42** Mt 9:27
[l]42 *Kristo* maana yake ni *Masiya*, yaani *Aliyetiwa mafuta.*
[m]**22:44** 1Fal 5:3; Ebr 1:13
[n]**22:46** Mk 12:34; Lk 20:40
[o]**23:1** Mk 12:38-40
[p]**23:2** Ezr 7:6, 25; Neh 8:4
[q]**23:3** Mal 2:7, 8
[r]**23:4** Mdo 15:10; Gal 6:13

lakini wao wenyewe hawako radhi hata
kuinua kidole ili kuisogeza.
5 [a]“Wao hutenda mambo yao yote ili
waonekane na watu. Hupanua vikasha vyao
vyenye maandiko ya sheria na kurefusha
matamvua ya mavazi yao. 6 [b]Wanapenda
kukalia viti vya heshima katika karamu, na
vile viti maalum sana katika masinagogi.
7 [c]Hupenda kusalimiwa masokoni na kutaka
watu wawaite ‘Rabi.’[d]
8 [e]“Lakini ninyi msiitwe ‘Rabi,’ kwa
sababu mnaye Bwana mmoja na ninyi nyote
ni ndugu. 9 [f]Nanyi msimwite mtu yeyote
‘Baba,’ hapa duniani, kwa maana mnaye
Baba mmoja, naye yuko mbinguni. 10 Wala
msiitwe ‘Mwalimu,’ kwa maana mnaye
mwalimu mmoja tu, ndiye Kristo.[g] 11 [h]Yeye
aliye mkuu kuliko ninyi nyote miongoni
mwenu atakuwa mtumishi wenu. 12 [i]Kwa
kuwa yeyote anayejikweza atashushwa, na
yeyote anayejinyenyekeza atakwezwa.
13 [j]“Lakini ole wenu, walimu wa sheria
na Mafarisayo, enyi wanafiki! Kwa maana
mnawafungia watu milango ya Ufalme wa
Mbinguni. Ninyi wenyewe hamuingii humo,
nao wale wanaotaka kuingia mnawazuia.
[ 14 [k]Ole wenu walimu wa sheria na
Mafarisayo, enyi wanafiki! Mnakula katika
nyumba za wajane, nanyi kwa kujifanya
kuwa wema, mnasali sala ndefu. Kwa hiyo
hukumu yenu itakuwa kuu zaidi.]
15 [l]“Ole wenu walimu wa sheria na
Mafarisayo, enyi wanafiki! Ninyi mnasafiri
baharini na nchi kavu ili kumfanya mtu
mmoja mwongofu, lakini baada ya
kumpata, mnamfanya mwana wa jehanamu
mara mbili kuliko ninyi!
16 [m]“Ole wenu, viongozi vipofu! Ninyi
mwasema, ‘Mtu akiapa kwa Hekalu,
kiapo hicho si kitu; lakini mtu akiapa kwa
dhahabu ya Hekalu, amefungwa kwa kiapo
chake.’ 17 [n]Ninyi vipofu wapumbavu! Ni kipi
kilicho kikuu zaidi: ni ile dhahabu, au ni
lile Hekalu linaloifanya hiyo dhahabu kuwa
takatifu? 18 Pia mnasema, ‘Mtu akiapa kwa
madhabahu, si kitu; lakini mtu akiapa kwa
sadaka iliyo juu ya madhabahu, amefungwa
kwa kiapo chake’ 19 [o]Ninyi vipofu! Ni kipi
kikuu zaidi: ni sadaka, au ni madhabahu
yanayoifanya hiyo sadaka kuwa takatifu?
20 Kwa hiyo, mtu aapaye kwa madhabahu,
huapa kwa hayo madhabahu na vitu vyote
vilivyo juu yake. 21 [p]Naye mtu aapaye kwa
Hekalu, huapa kwa hilo Hekalu na kwa
huyo akaaye ndani yake. 22 [q]Naye aapaye
kwa mbingu, huapa kwa kiti cha enzi cha
Mungu na kwa yeye aketiye juu ya kiti
hicho.
23 [r]“Ole wenu walimu wa sheria na
Mafarisayo, ninyi wanafiki! Kwa maana
mnatoa zaka ya mnanaa, bizari na jira,
lakini mmeacha mambo makuu zaidi ya
sheria, yaani haki, huruma na uaminifu.
Iliwapasa kufanya haya makuu ya sheria
bila kupuuza hayo matoleo. 24 [s]Ninyi
viongozi vipofu, mnachuja kiroboto lakini
mnameza ngamia!
25 [t]“Ole wenu, walimu wa sheria na
Mafarisayo, ninyi wanafiki! Kwa maana
mnasafisha kikombe na sahani kwa nje,
lakini ndani mmejaa unyang’anyi na
kutokuwa na kiasi. 26 [u]Ewe Farisayo kipofu!
Safisha ndani ya kikombe na sahani kwanza,
ndipo nje itakuwa safi pia.
27 [v]“Ole wenu, walimu wa sheria na
Mafarisayo, ninyi wanafiki! Mnafanana
na makaburi yaliyopakwa chokaa, ambayo

---

[a]**23:5** Mt 6:1-5, 16; Kut 13:6-9; Hes 15:38; Kum 22:12
[b]**23:6** Lk 14:7; 20:46
[c]**23:7** Mk 9:5; Yn 20:16
[d]7 Rabi maana yake Bwana, Mwalimu.
[e]**23:8** Yak 3:1; 2Kor 1:24; 1Pet 5:3
[f]**23:9** Mal 1:6; Mt 9:6
[g]10 *Kristo* maana yake ni *Masiya*, yaani *Aliyetiwa mafuta.*
[h]**23:11** Mt 20:26; Mk 9:35
[i]**23:12** Za 18:27; Lk 1:52
[j]**23:13** Mt 23:25-29; Lk 11:52
[k]**23:14** Mk 12:40; Lk 20:47; 2Tim 3:6; Tit 1:11
[l]**23:15** Mdo 6:5; 13:43; Mt 5:22
[m]**23:16** Isa 9; 16; Mt 15:14; 5:33-35
[n]**23:17** Kut 30:29
[o]**23:19** Kut 29:37
[p]**23:21** 1Fal 8:13; Za 26:8
[q]**23:22** Za 11:4; Mt 5:34
[r]**23:23** Law 27:30; Mik 6:8; Lk 11:42
[s]**23:24** Mt 23:16
[t]**23:25** Mk 7:4; Lk 11:39
[u]**23:26** Tit 1:15; Yn 9:40
[v]**23:27** Lk 11:44; Mdo 23:3

yanapendeza kwa nje, lakini ndani yamejaa
mifupa ya wafu na kila aina ya uchafu.
28 [a]Vivyo hivyo, kwa nje ninyi mnaonekana
kwa watu kuwa wenye haki, lakini kwa
ndani mmejaa unafiki na uovu.
29 [b]"Ole wenu, walimu wa sheria na
Mafarisayo, ninyi wanafiki! Mnajenga
makaburi ya manabii na kuyapamba
makaburi ya wenye haki. 30 Nanyi mwasema,
'Kama tungaliishi wakati wa baba zetu,
tusingalikuwa tumeshiriki katika kumwaga
damu ya manabii!' 31 [c]Hivyo mnajishuhudia
wenyewe kwamba ninyi ni wana wa wale
waliowaua manabii. 32 [d]Haya basi, kijazeni
kipimo cha dhambi ya baba zenu!
33 [e]"Ninyi nyoka, ninyi uzao wa nyoka
wenye sumu! Mtaiepukaje hukumu ya
jehanamu? 34 [f]Kwa sababu hii, tazameni,
natuma kwenu manabii na wenye hekima
na walimu. Baadhi yao mtawaua na
kuwasulubisha, na wengine wao mtawapiga
mijeledi katika masinagogi yenu na
kuwafuatia kutoka mji mmoja hadi mji
mwingine. 35 [g]Hivyo ile damu ya wenye
haki wote iliyomwagwa hapa duniani,
tangu damu ya Abeli, ambaye alikuwa hana
hatia, hadi damu ya Zekaria mwana wa
Barakia, mliyemuua kati ya patakatifu na
madhabahu, itawajia juu yenu. 36 [h]Amin,
nawaambia, haya yote yatakuja juu ya
kizazi hiki.

*Yesu Aililia Yerusalemu*

**(Luka 13:34-35)**

37 [i]"Ee Yerusalemu, Yerusalemu,
uwauaye manabii na kuwapiga mawe
wale waliotumwa kwako! Mara ngapi
nimetamani kuwakusanya watoto wako
pamoja, kama vile kuku akusanyavyo
vifaranga wake chini ya mabawa yake,
lakini hukutaka! 38 [j]Tazama nyumba
yenu imeachwa ukiwa. 39 [k]Kwa maana
nawaambia, hamtaniona tena tangu sasa
mpaka mtakaposema, 'Amebarikiwa yeye
ajaye kwa Jina la Bwana.' "

*Kubomolewa Kwa Hekalu Kwatabiriwa*

**(Marko 13:1-2; Luka 21:5-6)**

24 [l]Yesu akatoka Hekaluni na alipokuwa
akienda zake, wanafunzi wake
wakamwendea ili kumwonyesha majengo
ya Hekalu. 2 [m]Ndipo Yesu akawauliza, "Je,
mnayaona haya yote? Amin, nawaambia,
hakuna hata jiwe moja hapa litakalobaki
juu ya jingine, bali kila moja litabomolewa."

*Ishara Za Nyakati Za Mwisho*

**(Marko 13:3-23; Luka 21:7-24)**

3 [n]Yesu alipokuwa ameketi kwenye Mlima
wa Mizeituni, wanafunzi wake wakamjia
faraghani, wakamuuliza, "Tuambie, mambo
haya yatatukia lini, nayo dalili ya kuja
kwako na ya mwisho wa dunia ni gani?"
4 [o]Yesu akawajibu, "Jihadharini, mtu
yeyote asiwadanganye. 5 [p]Kwa maana wengi
watakuja kwa Jina langu, wakidai, 'Mimi
ndiye Kristo,'[q] nao watawadanganya wengi.
6 [r]Mtasikia habari za vita na matetesi ya
vita. Angalieni msitishike, kwa maana
haya hayana budi kutukia. Lakini ule
mwisho bado. 7 [s]Taifa litainuka dhidi ya
taifa, na ufalme dhidi ya ufalme. Kutakuwa
na njaa na mitetemeko ya ardhi sehemu
mbalimbali. 8 Haya yote yatakuwa ndio
mwanzo wa utungu.
9 [t]"Ndipo mtasalitiwa, ili mteswe na
kuuawa, nanyi mtachukiwa na mataifa

---

[a]**23:28** Lk 16:15
[b]**23:29** Lk 11:47-48
[c]**23:31** Mt 5:12; Mdo 7:51-52
[d]**23:32** 1The 2:16; Eze 20:4
[e]**23:33** Mt 3:7; 12:34; 5:22
[f]**23:34** 2Nya 36:15-16; Lk 11:49; Mt 10:17; 10:23
[g]**23:35** Mwa 4:8; Ebr 11:4; 2Nya 24:21
[h]**23:36** Mt 24:34; Lk 11:50-51
[i]**23:37** 2Nya 24:21; Mt 5:12
[j]**23:38** 1Fal 9:7-8; Yer 22:5
[k]**23:39** Za 118:26; Mt 21:9
[l]**24:1** Mk 13:1; Lk 21:5
[m]**24:2** Lk 19:44; 1Fal 9:7; Yer 26:18; Mik 3:12
[n]**24:3** Mt 21:1
[o]**24:4** Efe 5:6; Kol 2:8, 18; 2The 2:3; 1Yn 4:1
[p]**24:5** Mt 24:11, 23-24; 1Yn 2:18
[q]5 *Kristo* maana yake ni *Masiya*, yaani *Aliyetiwa mafuta.*
[r]**24:6** Dan 2:26
[s]**24:7** Isa 19:2; Mdo 11:28
[t]**24:9** Mt 10:17; Yn 16:2

yote kwa ajili yangu. 10 [a]Wakati huo, wengi
wataacha imani yao, nao watasalitiana
kila mmoja na mwenzake na kuchukiana.
11 [b]Watatokea manabii wengi wa uongo,
nao watawadanganya watu wengi. 12 Kwa
sababu ya kuongezeka kwa uovu upendo
wa watu wengi utapoa, 13 [c]lakini yule
atakayevumilia hadi mwisho ataokolewa.
14 [d]Injili ya Ufalme itahubiriwa ulimwenguni
kote kuwa ushuhuda kwa mataifa yote.
Ndipo mwisho utakapokuja.

15 [e]"Hivyo mtakapoona lile 'chukizo la
uharibifu' lililonenwa na nabii Danieli
limesimama mahali patakatifu (asomaye
na afahamu), 16 basi wale walioko Uyahudi
wakimbilie milimani. 17 [f]Yeyote aliye juu
ya dari ya nyumba asishuke ili kuchukua
chochote kutoka ndani ya nyumba. 18 Aliye
shambani asirudi nyumbani kuchukua
vazi lake. 19 [g]Ole wao wenye mimba na
wale wanaonyonyesha watoto siku hizo!
20 [h]Ombeni ili kukimbia kwenu kusiwe
wakati wa baridi au siku ya Sabato.
21 [i]Kwa maana wakati huo kutakuwa
na dhiki kuu ambayo haijapata kuwako
tangu mwanzo wa dunia mpaka sasa: wala
haitakuwako tena kamwe. 22 [j]Kama siku
hizo zisingefupishwa, hakuna hata mtu
mmoja ambaye angeokoka. Lakini kwa ajili
ya wateule, siku hizo zitafupizwa. 23 [k]Wakati
huo kama mtu yeyote akiwaambia, 'Tazama,
Kristo huyu hapa!' Au, 'Kristo yuko kule,'
msisadiki. 24 [l]Kwa maana watatokea
makristo wa uongo na manabii wa uongo,
nao watafanya ishara kubwa na maajabu
mengi ili kuwapotosha, ikiwezekana, hata
wale wateule hasa. 25 Angalieni, nimekwisha
kuwaambia mapema.

26 "Kwa hiyo mtu yeyote akiwaambia,
'Yule kule nyikani,' msiende huko. Au
akisema, 'Yuko kwenye chumba,' msisadiki.
27 [m]Kwa maana kama vile umeme utokeavyo
mashariki na kuonekana hata magharibi,
ndivyo itakavyokuwa kuja kwake Mwana
wa Adamu. 28 [n]Kwa maana popote ulipo
mzoga, huko ndiko wakusanyikapo tai.

*Kuja Kwa Mwana Wa Adamu*

**(Marko 13:24-31; Luka 21:25-33)**

29 [o]"Mara baada ya dhiki ya siku zile,

" 'jua litatiwa giza,
nao mwezi hautatoa nuru yake;
nazo nyota zitaanguka kutoka
angani,
na nguvu za anga zitatikisika.'

30 [p]"Ndipo itakapotokea ishara ya Mwana
wa Adamu angani, na makabila yote ya
dunia yataomboleza. Nao watamwona
Mwana wa Adamu akija juu ya mawingu
ya angani, katika uwezo na utukufu mkuu.
31 [q]Naye atawatuma malaika zake kwa sauti
kuu ya tarumbeta, nao watawakusanya
wateule wake kutoka pande zote nne za
dunia, kutoka mwisho mmoja wa mbingu
hadi mwisho mwingine.

32 [r]"Basi jifunzeni somo hili kutokana na
mtini: Matawi yake yanapoanza kuchipua na
kutoa majani, mnatambua kwamba wakati
wa kiangazi umekaribia. 33 [s]Vivyo hivyo,
myaonapo mambo haya yote, mnatambua
kwamba wakati u karibu, hata malangoni.
34 [t]Amin, nawaambia, kizazi hiki hakitapita
hadi mambo haya yote yawe yametimia.
35 [u]Mbingu na nchi zitapita, lakini maneno
yangu hayatapita kamwe.

---

[a]**24:10** Dan 11:41
[b]**24:11** Mt 7; 15
[c]**24:13** Mt 10:22
[d]**24:14** Mt 4:23; Rum 10:18; Ufu 3:10
[e]**24:15** Mdo 6:13; Dan 11:31; 12:11
[f]**24:17** 1Sam 9:25; Lk 12:3
[g]**24:19** Lk 23:29
[h]**24:20** Mdo 1:12
[i]**24:21** Eze 5:9; Dan 12:1
[j]**24:22** Isa 65:8, 9
[k]**24:23** Lk 17:23; 21:8
[l]**24:24** Kut 7:11, 22; Ufu 16:14
[m]**24:27** Lk 17:24; Mt 8:20
[n]**24:28** Lk 17:37
[o]**24:29** Sef 1:15; Ufu 8:12
[p]**24:30** Dan 7:13; Ufu 1:7
[q]**24:31** Mt 13:41; Zek 9:14; 1The 4:16
[r]**24:32** Lk 21:29
[s]**24:33** Yak 5:9
[t]**24:34** Mt 16:28; 23:36
[u]**24:35** Mt 5:18

*Hakuna Ajuaye Siku Wala Saa*

**(Marko 13:32-37; Luka 17:26-30, 34-36)**

36 [a]“Kwa habari ya siku ile na saa,
hakuna ajuaye, hata malaika walio
mbinguni wala Mwana, ila Baba peke
yake. 37 [b]Kama ilivyokuwa wakati wa
Noa, ndivyo itakavyokuwa kuja kwake
Mwana wa Adamu. 38 [c]Kwa maana siku
zile kabla ya gharika, watu walikuwa
wakila na kunywa, wakioa na kuolewa,
mpaka siku ile Noa alipoingia katika
safina. 39 [d]Nao hawakujua lolote mpaka
gharika ilipokuja ikawakumba wote. Hivyo
ndivyo itakavyokuwa atakapokuja Mwana
wa Adamu. 40 [e]Watu wawili watakuwa
shambani, naye mmoja atatwaliwa na
mwingine ataachwa. 41 [f]Wanawake wawili
watakuwa wanasaga pamoja, naye mmoja
atatwaliwa na mwingine ataachwa.

42 [g]“Basi kesheni, kwa sababu hamjui
ni siku gani atakapokuja Bwana wenu.
43 [h]Lakini fahamuni jambo hili: Kama
mwenye nyumba angejua ni wakati gani
wa usiku ambao mwizi atakuja, angekesha
na hangekubali nyumba yake kuvunjwa.
44 [i]Kwa hiyo ninyi pia hamna budi kuwa
tayari, kwa sababu Mwana wa Adamu
atakuja saa msiyotazamia.

*Mfano Wa Mtumishi Mwaminifu*

**(Luka 12:41-48)**

45 [j]“Ni nani basi aliye mtumishi
mwaminifu na mwenye busara, ambaye
bwana wake amemweka kusimamia
watumishi wengine katika nyumba yake, ili
awape chakula chao kwa wakati unaofaa?
46 [k]Heri mtumishi yule ambaye bwana wake
atakaporudi atamkuta akifanya hivyo.
47 [l]Amin, nawaambia, atamweka mtumishi
huyo kuwa msimamizi wa mali yake yote.
48 [m]Lakini kama huyo mtumishi ni mwovu,
naye akasema moyoni mwake, ‘Bwana
wangu atakawia muda mrefu,’ 49 [n]kisha
akaanza kuwapiga watumishi wenzake, na
kula na kunywa pamoja na walevi. 50 Basi
bwana wa mtumishi huyo atakuja siku
asiyodhani na saa asiyoijua. 51 [o]Atamkata
vipande vipande na kumweka katika
sehemu moja pamoja na wanafiki, mahali
ambako kutakuwa ni kulia na kusaga meno.

*Mfano Wa Wanawali Kumi*

25 [p]“Wakati huo, Ufalme wa Mbinguni
utakuwa kama wanawali kumi
waliochukua taa zao na kwenda kumlaki
bwana arusi. 2 [q]Watano wao walikuwa
wapumbavu na watano walikuwa wenye
busara. 3 Wale wapumbavu walichukua taa
zao lakini hawakuchukua mafuta ya akiba,
4 lakini wale wenye busara walichukua taa
zao na mafuta ya akiba kwenye vyombo.
5 [r]Bwana arusi alipokawia kuja wale
wanawali wote wakasinzia na kulala.

6 [s]“Usiku wa manane pakawa na kelele:
‘Tazameni, huyu hapa bwana arusi! Tokeni
nje mkamlaki!’

7 [t]“Ndipo wale wanawali wote wakaamka
na kuzitengeneza taa zao. 8 [u]Wale
wapumbavu wakawaambia wale wenye
busara, ‘Tupatieni mafuta yenu kidogo;
taa zetu zinazimika.’

9 “Lakini wale wenye busara wakawajibu,
‘Sivyo, hayatutoshi sisi na ninyi pia. Afadhali
mwende kwa wauzao mkajinunulie mafuta
yenu.’

10 [v]“Nao walipokuwa wakienda kununua
mafuta, bwana arusi akafika. Wale wanawali

---

[a]**24:36** Mdo 1:7
[b]**24:37** Mwa 6:5; 7:6-23
[c]**24:38** Mt 22:30
[d]**24:39** Lk 15
[e]**24:40** Lk 17:34-35
[f]**24:41** Lk 17:30
[g]**24:42** Mt 25:13; Lk 12:40
[h]**24:43** Lk 12:39
[i]**24:44** 1The 5:6
[j]**24:45** Mt 25:21-23
[k]**24:46** Ufu 16:15
[l]**24:47** Mt 25:21, 23; Lk 22:29
[m]**24:48** Mhu 8:11
[n]**24:49** Lk 21:34
[o]**24:51** Mt 8:12
[p]**25:1** Mt 13:24; Mdo 20:8; Ufu 4:5; 19:7; 21:2
[q]**25:2** Mt 24:45
[r]**25:5** 1The 5:6
[s]**25:6** Mt 24:31; 1The 3
[t]**25:7** Lk 12:35
[u]**25:8** Lk 12:35
[v]**25:10** Ufu 19:9

waliokuwa tayari wakaingia ndani pamoja
naye kwenye karamu ya arusi na mlango
ukafungwa.
11 [a]“Baadaye wale wanawali wengine
nao wakaja, wakaita, ‘Bwana! Bwana!
Tufungulie mlango!’
12 [b]“Lakini yeye bwana arusi akawajibu,
‘Amin, amin nawaambia, siwajui ninyi!’
13 [c]“Kwa hiyo kesheni, kwa sababu hamjui
siku wala saa.

*Mfano Wa Watumishi Watatu Na Talanta*

**(Luka 19:11-27)**

14 [d]“Tena, Ufalme wa Mbinguni ni kama
mtu aliyetaka kusafiri, naye akawaita
watumishi wake na kuweka mali yake
kwenye uangalizi wao. 15 [e]Mmoja akampa
talanta[f] tano, mwingine talanta mbili, na
mwingine talanta moja. Kila mmoja alipewa
kwa kadiri ya uwezo wake. Kisha yeye
akasafiri. 16 Yule aliyepewa talanta tano
akaenda mara moja akafanya nazo biashara
akapata talanta nyingine tano zaidi. 17 Yule
aliyepewa talanta mbili akafanya vivyo
hivyo, akapata nyingine mbili zaidi. 18 Lakini
yule mtumishi aliyekuwa amepokea talanta
moja, alikwenda akachimba shimo ardhini
na kuificha ile fedha ya bwana wake.
19 [g]“Baada ya muda mrefu, yule bwana
wa wale watumishi akarudi na kufanya
hesabu nao. 20 Yule mtumishi aliyepokea
talanta tano akaja, akaleta nyingine tano
zaidi. Akasema, ‘Bwana uliweka kwenye
uangalizi wangu talanta tano. Tazama,
nimepata faida ya talanta tano zaidi.’
21 [h]“Bwana wake akamwambia,
‘Umefanya vizuri sana, mtumishi mwema
na mwaminifu! Umekuwa mwaminifu kwa
vitu vichache; nami nitakuweka kuwa
msimamizi wa vitu vingi. Njoo ushiriki
katika furaha ya bwana wako!’
22 “Yule mwenye talanta mbili naye
akaja. Akasema, ‘Bwana, uliweka kwenye
uangalizi wangu talanta mbili. Tazama
nimepata hapa talanta mbili zaidi.’
23 [i]“Bwana wake akajibu, ‘Umefanya
vizuri sana, mtumishi mwema na
mwaminifu. Umekuwa mwaminifu kwa
vitu vichache; nami nitakuweka kuwa
msimamizi wa vitu vingi. Njoo ushiriki
katika furaha ya bwana wako!’
24 “Kisha yule mtumishi aliyepokea
talanta moja akaja, akasema, ‘Bwana, nilijua
kwamba wewe ni mtu mgumu, unayevuna
mahali usipopanda na kukusanya mahali
usipotawanya mbegu. 25 Kwa hiyo niliogopa,
nikaenda, nikaificha talanta yako ardhini.
Tazama, hii hapa ile iliyo mali yako.’
26 “Bwana wake akajibu, ‘Wewe mtumishi
mwovu na mvivu! Ulijua kwamba ninavuna
mahali nisipopanda na kukusanya mahali
nisipotawanya mbegu. 27 Vyema basi,
ingekupasa kuweka fedha yangu kwa watoa
riba, ili nirudipo, nichukue ile iliyo yangu
na faida yake.
28 “ ‘Basi mnyang’anyeni hiyo talanta,
mkampe yule mwenye talanta kumi. 29 [j]Kwa
maana kila mtu aliye na kitu atapewa
zaidi, naye atakuwa navyo tele. Lakini
yule asiye na kitu, hata kile alicho nacho
atanyang’anywa. 30 [k]Nanyi mtupeni huyo
mtumishi asiyefaa nje, kwenye giza, mahali
ambako kutakuwa na kilio na kusaga meno.’

*Kondoo Na Mbuzi*

31 [l]“Mwana wa Adamu atakapokuja katika
utukufu wake na malaika wote watakatifu
pamoja naye, ndipo atakapoketi juu ya
kiti cha enzi cha utukufu wake. 32 [m]Mataifa
yote watakusanyika mbele zake, naye
atawatenga kama mchungaji anavyotenga
kondoo na mbuzi. 33 [n]Atawaweka kondoo
upande wake wa kuume, na mbuzi upande
wake wa kushoto.

---

[a]**25:11** Lk 13:25, 27; Mt 7:21; 2:23
[b]**25:12** Mt 7:23; Za 5:5; Hab 1:12; Yn 9:31
[c]**25:13** Mk 13:35; Lk 12:40
[d]**25:14** Mt 21:33; Lk 19:21
[e]**25:15** Mt 18:24-25
[f]15 Talanta moja ilikuwa sawa na mshahara wa kibarua wa miaka 15.
[g]**25:19** Mt 18:23
[h]**25:21** Mt 24:45-47; Lk 16:10
[i]**25:23** Mt 25:21
[j]**25:29** Mk 4:25; Lk 19:26
[k]**25:30** Mt 8:12
[l]**25:31** Mt 16:27; Lk 17:30; Mt 19:28
[m]**25:32** Mal 3:18; Eze 34:17-20
[n]**25:33** Eze 34:17

34 [a]“Ndipo Mfalme atawaambia wale
walioko upande wake wa kuume, ‘Njooni,
ninyi mliobarikiwa na Baba yangu; urithini
Ufalme ulioandaliwa kwa ajili yenu
tangu kuumbwa kwa ulimwengu. 35 [b]Kwa
maana nilikuwa na njaa mkanipa chakula,
nilikuwa na kiu mkaninywesha, nilikuwa
mgeni mkanikaribisha, 36 [c]nilikuwa
uchi mkanivika, nilikuwa mgonjwa
mkanitunza, nami nilikuwa kifungoni
mkaja kunitembelea.’
37 [d]“Ndipo wale wenye haki
watakapomjibu, ‘Bwana, ni lini tulikuona
ukiwa na njaa tukakulisha, au ukiwa na kiu
tukakunywesha? 38 Lini tulikuona ukiwa
mgeni tukakukaribisha, au ukiwa uchi
tukakuvika? 39 Tena ni lini tulikuona ukiwa
mgonjwa tukakutunza, au ukiwa kifungoni
tukakutembelea?’
40 [e]“Naye Mfalme atawajibu, ‘Amin
nawaambia, kwa jinsi mlivyomtendea
mmojawapo wa hawa ndugu zangu walio
wadogo, mlinitendea mimi.’
41 [f]“Kisha atawaambia wale walio upande
wake wa kushoto, ‘Ondokeni kwangu,
ninyi mliolaaniwa, nendeni kwenye moto
wa milele ulioandaliwa kwa ajili ya ibilisi
na malaika zake. 42 Kwa maana nilikuwa
na njaa hamkunipa chakula, nilikuwa
na kiu hamkuninywesha, 43 nilikuwa
mgeni nanyi hamkunikaribisha, nilikuwa
uchi hamkunivika, nilikuwa mgonjwa
hamkunitunza, na nilikuwa gerezani nanyi
hamkuja kunitembelea.’
44 “Ndipo wao pia watajibu, ‘Bwana ni
lini tulikuona ukiwa na njaa au kiu, au
ukiwa mgeni au uchi, au ukiwa mgonjwa
na kifungoni na hatukukuhudumia?’
45 [g]“Naye atawajibu, ‘Amin nawaambia,
kwa jinsi ambavyo hamkumtendea
mmojawapo wa hawa ndugu zangu walio
wadogo, hamkunitendea mimi.’
46 [h]“Ndipo hawa watakapoingia kwenye
adhabu ya milele, lakini wale wenye haki
wataingia katika uzima wa milele.”

*Shauri Baya La Kumuua Yesu*

**(Marko 14:1-2; Luka 22:1-2; Yohana 11:45-53)**

26 [i]Yesu alipomaliza kusema hayo
yote, akawaambia wanafunzi wake,
2 [j]“Kama mnavyojua, baada ya siku mbili
itakuwa Pasaka, naye Mwana wa Adamu
atasalitiwa ili asulubiwe.”
3 [k]Basi viongozi wa makuhani na wazee
wa watu wakakusanyika katika jumba la
utawala la kuhani mkuu, jina lake Kayafa.
4 [l]Wakafanya shauri ili kumkamata Yesu
kwa siri na kumuua. 5 [m]Lakini wakasema,
“Isiwe wakati wa Sikukuu, kusitokee ghasia
miongoni mwa watu.”

*Yesu Anapakwa Mafuta Huko Bethania*

**(Marko 14:3-9; Yohana 12:1-8)**

6 [n]Yesu alikuwa Bethania nyumbani
mwa Simoni aliyekuwa na ukoma, 7 naye
mwanamke mmoja akamjia akiwa na chupa
ya marhamu yenye manukato ya thamani
kubwa; akayamimina kichwani mwa Yesu
alipokuwa ameketi mezani kula chakula.
8 [o]Lakini wanafunzi wake walipoona
hayo wakakasirika, wakasema, “Upotevu
huu wote ni wa nini? 9 Manukato haya
yangeuzwa kwa bei kubwa, na fedha hizo
wakapewa maskini.”
10 [p]Yesu, akijua jambo hili, akawaambia,
“Mbona mnamsumbua huyu mwanamke?
Yeye amenitendea jambo zuri sana.
11 [q]Maskini mtakuwa nao siku zote,
lakini mimi hamtakuwa nami siku zote.
12 [r]Alipomiminia haya manukato kwenye

---

[a]**25:34** Gal 5:21; Yak 2:5; Ebr 9:26; Ufu 17:8
[b]**25:35** Isa 58:7; Ebr 13:2
[c]**25:36** Eze 18:7; Yak 2:15-16; 1:17; 2Tim 1:16
[d]**25:37** Mt 6:3
[e]**25:40** Mit 19:17; Ebr 6:10
[f]**25:41** Mt 7:23; Isa 66:24; 2Pet 2:4; Lk 3:17
[g]**25:45** Mit 14:31; 17:5
[h]**25:46** Gal 6:8; 1Yn 1:2; Dan 12:2; Yn 5:29
[i]**26:1** Mt 7:28
[j]**26:2** Yn 11:55; 13:1
[k]**26:3** Za 2:2; Lk 3:2; Mdo 4:6
[l]**26:4** Mt 12:14
[m]**26:5** Mt 27:24
[n]**26:6** Mt 21:17
[o]**26:8** Yn 12:4
[p]**26:10** Lk 11:7
[q]**26:11** Kum 15:11
[r]**26:12** Yn 19:40

mwili wangu, amefanya hivyo ili kuniandaa
kwa ajili ya maziko yangu. 13 Amin,
nawaambia, mahali popote ulimwenguni
ambapo hii Injili itahubiriwa, jambo hili
alilolitenda huyu mwanamke litatajwa pia
kwa ukumbusho wake."

*Yuda Akubali Kumsaliti Yesu*

**(Marko 14:10-11; Luka 22:3-6)**

14 [a]Kisha mmojawapo wa wale kumi na
wawili, aitwaye Yuda Iskariote, alikwenda
kwa viongozi wa makuhani 15 [b]na kuuliza,
"Mtanipa nini nikimtia Yesu mikononi
mwenu?" Wakamlipa vipande thelathini
vya fedha. 16 [c]Tangu wakati huo Yuda akawa
anatafuta wakati uliofaa wa kumsaliti Yesu.

*Yesu Ala Pasaka Pamoja Na Wanafunzi*

**(Marko 14:12-21; Luka 22:7-23; Yohana 13:21-30)**

17 [d]Siku ya kwanza ya Sikukuu ya Mikate
Isiyotiwa Chachu, wanafunzi walimjia Yesu
wakamuuliza, "Unataka twende wapi ili
tukuandalie mahali pa kula Pasaka?"
18 [e]Akajibu, "Nendeni kwa mtu fulani
huko mjini, mkamwambie, 'Mwalimu asema
hivi: Saa yangu imekaribia. Nitaiadhimisha
Pasaka pamoja na wanafunzi wangu katika
nyumba yako.' " 19 Hivyo wanafunzi
wakafanya kama vile Yesu alivyokuwa
amewaelekeza, nao wakaandaa Pasaka.
20 [f]Ilipofika jioni, Yesu alikuwa ameketi
mezani pamoja na wale wanafunzi wake
kumi na wawili. 21 [g]Nao walipokuwa wakila,
Yesu akasema, "Amin, nawaambia, mmoja
wenu atanisaliti."
22 Wakahuzunika sana, wakaanza
kumuuliza mmoja baada ya mwingine, "Je,
ni mimi Bwana?"
23 [h]Yesu akawaambia, "Yule aliyechovya
mkono wake katika bakuli pamoja nami
ndiye atakayenisaliti. 24 [i]Mwana wa Adamu
anaenda zake kama vile alivyoandikiwa.
Lakini ole wake mtu yule amsalitiye Mwana
wa Adamu. Ingekuwa heri kwake mtu huyo
kama hangezaliwa!"
25 [j]Kisha Yuda, yule mwenye kumsaliti,
akasema, "Je, ni mimi Rabi?"
Yesu akajibu, "Naam, wewe mwenyewe
umesema."

*Kuanzishwa Kwa Meza Ya Bwana*

**(Marko 14:22-26; Luka 22:14-20; 1 Wakorintho 11:23-25)**

26 [k]Walipokuwa wanakula, Yesu
akachukua mkate, akashukuru, akaumega,
na kuwapa wanafunzi wake, akisema,
"Twaeni, mle; huu ndio mwili wangu."
27 [l]Kisha akakitwaa kikombe, akashukuru,
akawapa, akisema, "Nyweni nyote katika
kikombe hiki. 28 [m]Hii ndiyo damu yangu ya
Agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa
ondoleo la dhambi. 29 [n]Lakini ninawaambia,
tangu sasa sitakunywa tena katika uzao huu
wa mzabibu, hadi siku ile nitakapounywa
mpya pamoja nanyi katika Ufalme wa Baba
yangu."
30 [o]Walipokwisha kuimba wimbo,
wakatoka wakaenda Mlima wa Mizeituni.

*Yesu Atabiri Petro Kumkana*

**(Marko 14:27-31; Luka 22:31-34; Yohana 13:36-38)**

31 [p]Kisha Yesu akawaambia, "Usiku
huu, ninyi nyote mtaniacha, kwa maana
imeandikwa:

" 'Nitampiga mchungaji,
nao kondoo wa hilo kundi
watatawanyika.'

32 [q]Lakini baada ya kufufuka kwangu,
nitawatangulia kwenda Galilaya."

---

[a]**26:14** Mt 26:25, 47; 10:4
[b]**26:15** Kut 21:32; Zek 11:12
[c]**26:16** 1Tim 6:9, 10
[d]**26:17** Kut 12:18-20
[e]**26:18** Mk 14:35, 41; Yn 17:1
[f]**26:20** Mk 14:17-21; Lk 22:14
[g]**26:21** Lk 22:21-23; Yn 13:21
[h]**26:23** Za 41:9; Yn 13:18
[i]**26:24** Dan 9:24; 1Pet 1:10-11
[j]**26:25** Mt 23:7
[k]**26:26** Mt 14:9; 1Kor 10:16
[l]**26:27** Mk 14:23
[m]**26:28** Mal 2:5; Ebr 10:29; Mt 20:28; Mk 1:4
[n]**26:29** Mdo 10:41
[o]**26:30** Mt 21:1; Mk 14:26
[p]**26:31** Mt 11:6; 13:21; Zek 13:7; Yn 16:32
[q]**26:32** Mt 28:7, 10, 16

33 Petro akajibu, “Hata kama wote
watakuacha, kamwe mimi sitakuacha.”
34 [a]Yesu akamjibu, “Amin, nakuambia,
usiku huu, kabla jogoo hajawika, utanikana
mara tatu.”
35 [b]Lakini Petro akasisitiza, “Hata kama
itabidi kufa pamoja nawe, sitakukana
kamwe.” Nao wanafunzi wale wengine
wote wakasema vivyo hivyo.

*Yesu Anaomba Gethsemane*

**(Marko 14:32-42; Luka 22:39-46)**

36 [c]Kisha Yesu akaenda pamoja na
wanafunzi wake mpaka kwenye bustani
iitwayo Gethsemane, akawaambia, “Kaeni
hapa, nami niende kule nikaombe.”
37 [d]Akamchukua Petro pamoja na wale wana
wawili wa Zebedayo, akaanza kuhuzunika
na kufadhaika. 38 [e]Kisha Yesu akawaambia,
“Moyo wangu umejawa na huzuni kiasi cha
kufa. Kaeni hapa na mkeshe pamoja nami.”
39 [f]Akaenda mbele kidogo, akaanguka
kifudifudi, akaomba akisema, “Baba
yangu, kama inawezekana, kikombe hiki
na kiniondokee. Lakini si kama nipendavyo
mimi, bali kama upendavyo wewe.”
40 [g]Kisha akarudi kwa wanafunzi wake,
akawakuta wamelala. Akamuuliza Petro,
“Je, ninyi hamkuweza kukesha pamoja
nami hata kwa saa moja? 41 [h]Kesheni na
mwombe, msije mkaingia majaribuni. Roho
iko radhi, lakini mwili ni mdhaifu.”
42 [i]Akaenda tena mara ya pili na kuomba,
“Baba yangu, kama haiwezekani kikombe
hiki kiniepuke nisikinywe, basi mapenzi
yako yafanyike.”
43 Aliporudi, akawakuta tena wamelala
kwa sababu macho yao yalikuwa mazito.
44 [j]Hivyo akawaacha akaenda zake tena
mara ya tatu na kuomba akisema maneno
yale yale.
45 [k]Kisha akarudi kwa wanafunzi
wake, akawaambia, “Bado mmelala na
kupumzika? Tazameni, saa imefika ambapo
Mwana wa Adamu anasalitiwa na kutiwa
mikononi mwa wenye dhambi. 46 [l]Inukeni,
twende zetu! Tazameni, msaliti wangu
yuaja!”

*Yesu Akamatwa*

**(Marko 14:43-50; Luka 22:47-53; Yohana 18:3-12)**

47 [m]Alipokuwa bado anazungumza, Yuda,
mmoja wa wale Kumi na Wawili, akafika.
Alikuwa amefuatana na umati mkubwa wa
watu wenye panga na marungu, waliokuwa
wametumwa na viongozi wa makuhani na
wazee wa watu. 48 Basi msaliti alikuwa
amewapa hao watu ishara, kwamba: “Yule
nitakayembusu ndiye. Mkamateni.” 49 [n]Mara
Yuda akamjia Yesu na kumsalimu, “Salamu,
Rabi!” Akambusu.
50 [o]Yesu akamwambia, “Rafiki, fanya kile
ulichokuja kufanya hapa.”
Kisha wale watu wakasogea mbele,
wakamkamata Yesu. 51 [p]Ghafula mmoja wa
wale waliokuwa na Yesu alipoona hivyo,
akaushika upanga wake, akauchomoa
na kumpiga mtumishi wa kuhani mkuu,
akamkata sikio.
52 [q]Ndipo Yesu akamwambia, “Rudisha
upanga wako mahali pake, kwa maana
wote watumiao upanga watakufa kwa
upanga. 53 [r]Je, unadhani siwezi kumwomba
Baba yangu naye mara moja akaniletea
zaidi ya majeshi kumi na mawili ya
malaika? 54 [s]Lakini je, yale Maandiko
yanayotabiri kwamba ni lazima itendeke
hivi yatatimiaje?”

---

[a]**26:34** Yn 13:38
[b]**26:35** Yn 13:37
[c]**26:36** Mk 14:32, 35; Lk 22:39; Yn 18:1
[d]**26:37** Mt 4:21
[e]**26:38** Yn 12:27
[f]**26:39** Mt 20:22; Za 40:6-8; Yn 4:34
[g]**26:40** Mt 26:38
[h]**26:41** Mt 6:13
[i]**26:42** Mt 26:39
[j]**26:44** 2Kor 12:8
[k]**26:45** Mt 26:18
[l]**26:46** Yn 14:31
[m]**26:47** Mt 10:4
[n]**26:49** Mt 23:7
[o]**26:50** Mt 20:13; 22:12
[p]**26:51** Lk 22:36-38; Yn 18:10
[q]**26:52** Kut 21:12; Ufu 13:10
[r]**26:53** 2Fal 6:17; Mt 4:11
[s]**26:54** Mt 1:22; 26:24

55 [a]Wakati huo, Yesu akawaambia ule
umati wa watu, "Je, mmekuja na panga
na marungu kunikamata kana kwamba
mimi ni mnyang'anyi? Siku kwa siku
niliketi Hekaluni nikifundisha, mbona
hamkunikamata? 56 [b]Lakini haya yote
yametukia ili maandiko ya manabii yapate
kutimia." Ndipo wanafunzi wake wote
wakamwacha na kukimbia.

### *Yesu Mbele Ya Kuhani Mkuu*

**(Marko 14:53-65; Luka 22:54-71; Yohana 18:13-24)**

57 [c]Wale waliokuwa wamemkamata Yesu
wakampeleka kwa Kayafa, kuhani mkuu,
mahali ambapo walimu wa sheria pamoja na
wazee walikuwa wamekusanyika. 58 [d]Lakini
Petro akamfuata kwa mbali hadi uani kwa
kuhani mkuu. Akaingia ndani, akaketi
pamoja na walinzi ili aone litakalotukia.
59 [e]Viongozi wa makuhani na Baraza la
Wayahudi lote wakatafuta ushahidi wa
uongo dhidi ya Yesu ili wapate kumuua.
60 [f]Lakini hawakupata jambo lolote, ingawa
mashahidi wengi wa uongo walijitokeza.
Hatimaye wakajitokeza mashahidi
wawili wa uongo 61 [g]na kusema, "Huyu
mtu alisema, 'Ninaweza kulivunja Hekalu
la Mungu na kulijenga tena kwa siku tatu.' "
62 [h]Kisha kuhani mkuu akasimama na
kumwambia Yesu, "Je, wewe hutajibu? Ni
ushahidi gani hawa watu wanauleta dhidi
yako?" 63 [i]Lakini Yesu akakaa kimya.
Ndipo kuhani mkuu akamwambia,
"Nakuapisha mbele za Mungu aliye hai.
Tuambie kama wewe ndiwe Kristo,[j] Mwana
wa Mungu."
64 [k]Yesu akajibu, "Wewe umenena. Lakini
ninawaambia nyote: Siku za baadaye,
mtamwona Mwana wa Adamu akiwa
ameketi mkono wa kuume wa Mwenye
Nguvu, na akija juu ya mawingu ya
mbinguni."
65 [l]Ndipo kuhani mkuu akararua mavazi
yake na kusema, "Amekufuru! Tuna haja
gani tena ya mashahidi zaidi? Tazama, sasa
ninyi mmesikia hayo makufuru. 66 [m]Uamuzi
wenu ni gani?"
Wakajibu, "Anastahili kufa."
67 [n]Kisha wakamtemea mate usoni na
wengine wakampiga ngumi. Wengine
wakampiga makofi 68 [o]na kusema, "Tutabirie,
wewe Kristo! Ni nani aliyekupiga?"

### *Petro Amkana Bwana Yesu*

**(Marko 14:66-72; Luka 22:56-62; Yohana 18:15-18, 25-27)**

69 [p]Wakati huu Petro alikuwa amekaa nje
uani. Mtumishi mmoja wa kike akamjia na
kumwambia, "Wewe pia ulikuwa pamoja
na Yesu wa Galilaya."
70 Lakini Petro akakana mbele yao wote
akisema, "Sijui hilo usemalo."
71 Alipotoka nje kufika kwenye lango,
mtumishi mwingine wa kike alimwona,
akawaambia watu waliokuwepo, "Huyu
mtu alikuwa pamoja na Yesu, Mnazareti."
72 Akakana tena kwa kiapo akisema,
"Mimi simjui huyo!"
73 [q]Baada ya muda mfupi, wale waliokuwa
wamesimama pale wakamwendea Petro,
wakamwambia, "Hakika wewe ni mmoja
wao, kwa maana usemi wako ni kama wao."
74 [r]Ndipo Petro akaanza kujilaani na
kuwaapia, "Mimi simjui mtu huyo!"
Papo hapo jogoo akawika. 75 [s]Ndipo
Petro akakumbuka lile neno Yesu alilokuwa
amesema: "Kabla jogoo hajawika, utanikana
mara tatu." Naye akaenda nje, akalia kwa
majonzi.

---

[a]**26:55** Lk 21:27; Yn 18:20
[b]**26:56** Mt 26:31
[c]**26:57** Mk 14:53; Lk 22:54; Yn 18:12; 13:14
[d]**26:58** Mk 14:66; 15:16; Lk 22:55; 11:21
[e]**26:59** Mt 5:22
[f]**26:60** Za 27:12; Mdo 6:13; Kum 19:15
[g]**26:61** Yn 2:19
[h]**26:62** Mk 14:60
[i]**26:63** Mt 27:12-14; Mk 14:61; Dan 7:13
[j]63 *Kristo* maana yake ni *Masiya*, yaani *Aliyetiwa mafuta.*
[k]**26:64** Dan 7:13; Mt 16:27; 24:30; Lk 21:27
[l]**26:65** Mk 14:63
[m]**26:66** Law 24:16; Yn 19:7
[n]**26:67** Mt 16:21; 27:30
[o]**26:68** Lk 22:63-65
[p]**26:69** Mk 14:66; Lk 22:55; Yn 18:16, 17, 25
[q]**26:73** Lk 22:59
[r]**26:74** Mk 14:71
[s]**26:75** Mt 26:24; Yn 13:38

*Yesu Aletwa Mbele Ya Pilato*

**(Marko 15:1; Luka 23:1-2; Yohana 18:28-32)**

27 [a]Asubuhi na mapema, viongozi wa
makuhani wote na wazee wa watu
wakafanya shauri pamoja dhidi ya Yesu
ili kumuua. 2 [b]Wakamfunga, wakampeleka
na kumkabidhi kwa Pilato, ambaye alikuwa
mtawala wa Kirumi.

*Yuda Ajinyonga*

**(Matendo 1:18-19)**

3 [c]Yuda, ambaye alikuwa amemsaliti Yesu,
alipoona kuwa Yesu amehukumiwa, akajuta
na akarudisha vile vipande thelathini vya
fedha alivyopewa na viongozi wa makuhani
na wazee wa watu. 4 [d]Akasema, "Nimetenda
dhambi, kwa maana nimeisaliti damu isiyo
na hatia."

Wakamjibu, "Hilo latuhusu nini sisi? Ni
shauri yako."

5 [e]Basi Yuda akavitupa vile vipande vya
fedha ndani ya Hekalu akaondoka akaenda
kujinyonga.

6 [f]Wale viongozi wa makuhani
wakazichukua zile fedha wakasema, "Si
halali kuchanganya fedha hizi na sadaka
kwa sababu hizi ni fedha zenye damu."
7 Kwa hiyo baada ya kushauriana, waliamua
kuzitumia kununulia shamba la mfinyanzi,
liwe mahali pa kuzikia wageni. 8 [g]Hii ndiyo
sababu lile shamba likaitwa Shamba la
Damu hadi leo. 9 [h]Ndipo likatimia lile
lililonenwa na nabii Yeremia, kwamba,
"Walichukua vile vipande thelathini vya
fedha, thamani aliyopangiwa na watu
wa Israeli, 10 [i]wakanunulia shamba la
mfinyanzi, kama vile Bwana alivyoniagiza."

*Yesu Mbele Ya Pilato*

**(Marko 15:2-15; Luka 23:3-25; Yohana 18:33–19:16)**

11 [j]Wakati huo Yesu akiwa amesimama
mbele ya mtawala, mtawala akamuuliza,
"Wewe ndiye mfalme wa Wayahudi?"

Yesu akasema, "Wewe wasema hivyo."

12 [k]Lakini viongozi wa makuhani na wazee
walipomshtaki, hakujibu neno. 13 [l]Ndipo
Pilato akamuuliza, "Je, husikii ni mambo
mangapi wanayokushtaki nayo?" 14 [m]Lakini
Yesu hakumjibu hata kwa shtaka moja,
kiasi kwamba mtawala alishangaa sana.

15 [n]Basi ilikuwa ni desturi ya mtawala
kumfungua mfungwa mmoja aliyechaguliwa
na umati wa watu wakati wa sikukuu.
16 Wakati huo alikuwepo mfungwa mmoja
mwenye sifa mbaya, aliyeitwa Baraba.
17 [o]Hivyo umati wa watu walipokusanyika,
Pilato akawauliza, "Mnataka niwafungulie
nani, Baraba au Yesu yeye aitwaye Kristo?"
18 [p]Kwa kuwa alitambua Yesu alikuwa
amekabidhiwa kwake kwa ajili ya wivu.

19 [q]Pilato akiwa ameketi kwenye kiti cha
hukumu, mkewe akampelekea ujumbe huu:
"Usiwe na jambo lolote juu ya mtu huyu
asiye na hatia, kwa kuwa leo nimeteseka
sana katika ndoto kwa sababu yake."

20 [r]Lakini viongozi wa makuhani na wazee
wakaushawishi ule umati wa watu kwamba
waombe Baraba afunguliwe, naye Yesu
auawe.

21 Mtawala akawauliza tena, "Ni yupi kati
ya hawa wawili mnayetaka niwafungulie?"

Wakajibu, "Baraba."

22 [s]Pilato akawaambia, "Basi nifanye nini
na huyu Yesu aitwaye Kristo?"

Wakajibu wote, "Msulubishe!"

23 Pilato akauliza, "Kwa nini? Amefanya
kosa gani?"

[a]**27:1** Mk 15:1; Lk 22:66
[b]**27:2** Mt 20:19; Mdo 3:13; 1Tim 6:13
[c]**27:3** Mt 10:4; 26:14-15
[d]**27:4** Mt 27:24
[e]**27:5** Lk 1:9, 21; Mdo 1:18-19
[f]**27:6** Mk 12:41
[g]**27:8** Mdo 1:19
[h]**27:9** Mt 1:22
[i]**27:10** Zek 11:12-13; Yer 32:6-9
[j]**27:11** Mt 2:2
[k]**27:12** Mk 14:61; Yn 19:9
[l]**27:13** Mt 26:62
[m]**27:14** Mk 14:61
[n]**27:15** Yn 18:39
[o]**27:17** Mt 1:16
[p]**27:18** Yn 11:47, 48; 12:19
[q]**27:19** Yn 19:13; Mt 27:24; Hes 12:6
[r]**27:20** Mdo 3:14
[s]**27:22** Mt 1:16

Lakini wao wakazidi kupiga kelele,
wakisema, “Msulubishe!”
24 [a]Pilato alipoona kwamba hawezi
kufanya lolote, lakini badala yake ghasia
zilikuwa zinaanza, akachukua maji,
akanawa mikono yake mbele ya ule umati
wa watu, akasema, “Sina hatia juu ya damu
ya mtu huyu, hili ni jukumu lenu!”
25 [b]Watu wote wakajibu, “Damu yake na
iwe juu yetu na juu ya watoto wetu!”
26 [c]Basi akawafungulia Baraba. Lakini
baada ya kuamuru Yesu achapwe mijeledi,
akamtoa ili asulubishwe.

### *Askari Wamdhihaki Yesu*

**(Marko 15:16-20; Yohana 19:2-3)**

27 [d]Kisha askari wa mtawala wakampeleka
Yesu kwenye Praitorio[e] na wakakusanya
kikosi kizima cha askari kumzunguka.
28 [f]Wakamvua nguo zake na kumvika vazi
la rangi nyekundu, kisha 29 [g]wakasokota
taji ya miiba, wakaiweka kichwani pake.
Wakamwekea fimbo katika mkono wake wa
kuume, na wakapiga magoti mbele zake na
kumdhihaki, wakisema, “Salamu, mfalme
wa Wayahudi!” 30 [h]Wakamtemea mate,
wakachukua ile fimbo wakampiga kichwani
tena na tena. 31 [i]Baada ya kumdhihaki,
wakamvua lile joho, wakamvika tena
nguo zake. Kisha wakampeleka ili
wakamsulubishe.

### *Yesu Asulubishwa*

**(Marko 15:21-32; Luka 23:26-43; Yohana 19:17-27)**

32 [j]Walipokuwa wakienda, wakakutana
na mtu mmoja kutoka Kirene, jina lake
Simoni, nao wakamlazimisha kuubeba ule
msalaba. 33 [k]Wakafika mahali palipoitwa
Golgotha (maana yake ni Mahali pa
Fuvu la Kichwa). 34 [l]Hapo wakampa
Yesu divai iliyochanganywa na nyongo
ili anywe; lakini alipoionja, akakataa
kuinywa. 35 [m]Walipokwisha kumsulubisha
wakagawana mavazi yake kwa kuyapigia
kura. [Hili lilifanyika ili litimie lile neno
lililonenwa na nabii, “Waligawa nguo
zangu miongoni mwao na vazi langu
wakalipigia kura.”] 36 [n]Kisha wakaketi,
wakamchunga. 37 [o]Juu ya kichwa chake,
kwenye msalaba, wakaandika shtaka
lake hivi: HUYU NI YESU, MFALME WA
WAYAHUDI. 38 [p]Wanyang’anyi wawili
walisulubiwa pamoja naye, mmoja upande
wake wa kuume na mwingine upande wa
kushoto. 39 [q]Watu waliokuwa wakipita njiani
wakamtukana huku wakitikisa vichwa vyao
40 [r]na kusema, “Wewe ambaye utalivunja
Hekalu na kulijenga kwa siku tatu, jiokoe
mwenyewe basi! Kama wewe ni Mwana wa
Mungu, shuka kutoka msalabani.”
41 Vivyo hivyo, viongozi wa makuhani,
walimu wa sheria pamoja na wazee
wakamdhihaki wakisema, 42 [s]“Aliwaokoa
wengine, lakini hawezi kujiokoa mwenyewe!
Yeye ni Mfalme wa Israeli! Ashuke sasa
kutoka msalabani, nasi tutamwamini.
43 [t]Anamwamini Mungu, basi Mungu na
amwokoe sasa kama anamtaka, kwa maana
alisema, ‘Mimi ni Mwana wa Mungu.’ ”
44 [u]Hata wale wanyang’anyi waliosulubiwa
pamoja naye wakamtukana vivyo hivyo.

---

[a]**27:24** Mt 26:5; Za 26:6; Kum 21:6-8
[b]**27:25** Yos 2:19; Mdo 5:28
[c]**27:26** Isa 53:5; Yn 19:1
[d]**27:27** Yn 18:28-33; 19:9
[e]27 Praitorio maana yake ni makao makuu ya mtawala, jumba la kifalme lililokuwa linakaliwa na Pontio Pilato huko Yerusalemu, palipokuwa na kiti cha hukumu.
[f]**27:28** Yn 19:2
[g]**27:29** Isa 53:3; Yn 19:2-3
[h]**27:30** Mt 16:21; 26:27; 27:31; Isa 53:7
[i]**27:31** Mk 15:20-41; Lk 23:26
[j]**27:32** Ebr 13:12; Mdo 11:20; Mk 15:21; Lk 23:26
[k]**27:33** Yn 19:17
[l]**27:34** Mt 27:18; Za 69:21
[m]**27:35** Za 22:18
[n]**27:36** Mt 27:54
[o]**27:37** Mk 15:26; Lk 23:38; Yn 19:19
[p]**27:38** Isa 53:12
[q]**27:39** Za 109:25; Mao 2:15
[r]**27:40** Mt 26:61; Yn 2:19; Mt 4:3-6
[s]**27:42** Yn 1:49; 12:13; 3:15
[t]**27:43** Za 22:8
[u]**27:44** Mk 15:32; Lk 23:39

*Kifo Cha Yesu*

**(Marko 15:33-41; Luka 23:44-49;
Yohana 19:28-30)**

45 [a]Tangu saa sita hadi saa tisa giza
liliifunika nchi yote. 46 [b]Ilipofika saa tisa,
Yesu akapaza sauti akalia, *“Eloi, Eloi, lama
sabakthani?”* (maana yake, “Mungu wangu,
Mungu wangu, mbona umeniacha?”)

47 Baadhi ya watu waliokuwa
wamesimama pale waliposikia hayo,
wakasema, “Anamwita Eliya.”

48 [c]Ghafula mmoja wao akaenda mbio
na kuleta sifongo, akaichovya kwenye
siki, akaiweka kwenye mwanzi na akampa
Yesu ili anywe. 49 Wengine wakasema, “Basi
mwacheni. Hebu tuone kama Eliya atakuja
kumwokoa.”

50 [d]Yesu alipolia tena kwa sauti kuu,
akaitoa roho yake.

51 [e]Wakati huo huo pazia la Hekalu
likachanika vipande viwili, kuanzia juu
hadi chini. Dunia ikatetemeka na miamba
ikapasuka. 52 Makaburi yakafunguka na
miili ya watakatifu waliokuwa wamekufa
ikafufuliwa. 53 [f]Wakatoka makaburini, na
baada ya Yesu kufufuka, waliingia kwenye
Mji Mtakatifu na kuwatokea watu wengi.

54 [g]Basi yule jemadari na wale waliokuwa
pamoja naye wakimlinda Yesu walipoona
lile tetemeko na yale yote yaliyokuwa
yametukia, waliogopa, wakasema, “Hakika
huyu alikuwa Mwana wa Mungu!”

55 [h]Walikuwako wanawake huko
wakiangalia kwa mbali. Hawa walikuwa
wamemfuata Yesu tangu Galilaya ili
kushughulikia mahitaji yake. 56 [i]Miongoni
mwao walikuwepo Maria Magdalene, na
Maria mama yao Yakobo na Yosefu, na
mama yao wana wa Zebedayo.

*Maziko Ya Yesu*

**(Marko 15:42-47; Luka 23:50-56;
Yohana 19:38-42)**

57 [j]Ilipofika jioni, alifika mtu mmoja
tajiri kutoka Arimathaya aitwaye Yosefu,
ambaye pia alikuwa mwanafunzi wa Yesu.
58 Akamwendea Pilato ili kumwomba
mwili wa Yesu. Pilato akaamuru apewe.
59 Yosefu akauchukua mwili wa Yesu,
akaufunga katika kitambaa cha kitani
safi, 60 [k]na kuuweka katika kaburi lake
mwenyewe jipya, alilokuwa amelichonga
kwenye mwamba. Kisha akavingirisha jiwe
kubwa katika ingilio la kaburi, akaenda
zake. 61 Maria Magdalene na yule Maria
mwingine walikuwepo mahali pale, wakiwa
wameketi mkabala na kaburi.

*Walinzi Pale Kaburini*

62 Kesho yake, yaani siku iliyofuata ile
ya Maandalizi ya Sabato, viongozi wa
makuhani na Mafarisayo wakamwendea
Pilato 63 [l]na kusema, “Bwana, tumekumbuka
kwamba yule mdanganyifu wakati alikuwa
bado hai alisema, ‘Baada ya siku tatu
nitafufuka.’ 64 [m]Kwa hiyo uamuru kaburi
lilindwe kwa uthabiti mpaka baada ya siku
tatu. La sivyo, wanafunzi wake wanaweza
kuja kuuiba mwili wake na kuwaambia
watu kwamba amefufuliwa kutoka kwa
wafu. Udanganyifu huu wa mwisho
utakuwa mbaya kuliko ule wa kwanza.”

65 [n]Pilato akawaambia, “Ninyi mnao
askari walinzi. Nendeni, liwekeeni ulinzi
kadri mwezavyo.” 66 [o]Kwa hiyo wakaenda
na walinzi ili kulilinda kaburi kwa uthabiti,
wakatia muhuri kwenye lile jiwe na kuweka
ulinzi.

---

[a]**27:45** Amo 8:9
[b]**27:46** Za 22:1
[c]**27:48** Mt 27:34; Za 69:21
[d]**27:50** Yn 19:30
[e]**27:51** Kut 26:31-33; Ebr 10:19
[f]**27:53** Mt 4:5
[g]**27:54** Mt 4:3; 17:5
[h]**27:55** Lk 8:2-3
[i]**27:56** Lk 24:10; Yn 19:25
[j]**27:57** Kut 34:25; Mk 15:42; Lk 23:50; Yn 19:38
[k]**27:60** Mk 16:4; Mdo 13:29
[l]**27:63** Mt 16:21
[m]**27:64** Mt 28:13
[n]**27:65** Mt 28:11
[o]**27:66** Dan 6:7; Mt 28:2; 28:11

*Yesu Afufuka*

**(Marko 16:1-10; Luka 24:1-12;
Yohana 20:1-10)**

28 [a]Baada ya Sabato, alfajiri mapema siku
ya kwanza ya juma, Maria Magdalene
na yule Maria mwingine walikwenda
kulitazama kaburi.
2 [b]Ghafula, pakawa na tetemeko kubwa
la ardhi, kwa sababu malaika wa Bwana
alishuka kutoka mbinguni, akaenda penye
kaburi, akalivingirisha lile jiwe na kulikalia.
3 [c]Sura ya huyo malaika ilikuwa kama
umeme, na mavazi yake yalikuwa meupe
kama theluji. 4 Wale walinzi wa kaburi
walimwogopa sana, wakatetemeka hata
wakawa kama wafu.
5 [d]Yule malaika akawaambia wale
wanawake, “Msiogope, kwa maana ninajua
kuwa mnamtafuta Yesu aliyesulubiwa.
6 [e]Hayupo hapa, kwa kuwa amefufuka,
kama vile alivyosema. Njooni mpatazame
mahali alipokuwa amelazwa. 7 [f]Kisha
nendeni upesi mkawaambie wanafunzi
wake kwamba, ‘Amefufuka kutoka kwa
wafu, naye awatangulia kwenda Galilaya.
Huko ndiko mtamwona. Sasa nimekwisha
kuwaambia.’ ”
8 Hivyo wale wanawake wakaondoka pale
kaburini wakiwa wamejawa na hofu, bali
wakiwa na furaha nyingi. Wakaenda mbio
kuwaeleza wanafunzi wake habari hizo.
9 [g]Ghafula, Yesu akakutana nao, akasema,
“Salamu!” Wale wanawake wakamkaribia,
wakaishika miguu yake, wakamwabudu.
10 [h]Ndipo Yesu akawaambia, “Msiogope.
Nendeni mkawaambie ndugu zangu waende
Galilaya, ndiko watakakoniona.”

*Taarifa Ya Walinzi*

11 [i]Wakati wale wanawake walikuwa
njiani wakienda, baadhi ya wale askari
waliokuwa wakilinda kaburi walienda mjini
na kuwaeleza viongozi wa makuhani kila
kitu kilichokuwa kimetukia. 12 Baada ya
viongozi wa makuhani kukutana na wazee
na kutunga hila, waliwapa wale askari
kiasi kikubwa cha fedha 13 [j]wakiwaambia,
“Inawapasa mseme, ‘Wanafunzi wake
walikuja wakati wa usiku na kumwiba sisi
tulipokuwa tumelala.’ 14 [k]Kama habari hizi
zikimfikia mtawala, sisi tutamwondolea
mashaka nanyi hamtapata tatizo lolote.”
15 Kwa hiyo wale askari wakazipokea
hizo fedha nao wakafanya kama
walivyoelekezwa. Habari hii imeenea
miongoni mwa Wayahudi mpaka leo.

*Yesu Awatuma Wanafunzi Wake*

**(Marko 16:14-18; Luka 24:36-49;
Yohana 20:19-23; Matendo 1:6-8)**

16 [l]Basi wale wanafunzi kumi na mmoja
wakaenda hadi Galilaya kwenye ule
mlima ambao Yesu alikuwa amewaagiza.
17 Walipomwona, wakamwabudu; lakini
baadhi yao wakaona shaka. 18 [m]Yesu
akawajia na kusema, “Nimepewa mamlaka
yote mbinguni na duniani. 19 [n]Kwa sababu
hii, enendeni mkawafanye mataifa yote
kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa Jina
la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu,
20 [o]nanyi wafundisheni kuyashika mambo
yote niliyowaamuru ninyi. Hakika mimi
niko pamoja nanyi siku zote, hadi mwisho
wa nyakati.”

---

[a]**28:1** Mt 27:56
[b]**28:2** Mt 27:51; Yn 20:12; Mdo 5:9
[c]**28:3** Dan 7:9; Yn 20:12
[d]**28:5** Mt 14:27
[e]**28:6** Mt 16:21
[f]**28:7** Mt 26:32
[g]**28:9** Yn 20:14-18
[h]**28:10** Rum 8:29; Ebr 2:11-17
[i]**28:11** Mt 27:65-66
[j]**28:13** Mt 27:64
[k]**28:14** Mt 27:2
[l]**28:16** Mt 26:32
[m]**28:18** Dan 7:13, 14; Efe 1:20-22
[n]**28:19** Isa 49:6; Mdo 14:21
[o]**28:20** Mt 18:20; Yn 14:23

# MARKO

*Mahubiri Ya Yohana Mbatizaji*

**(Mathayo 3:1-12; Luka 3:1-8; Yohana 1:19-28)**

1 [a]Mwanzo wa Injili ya Yesu Kristo, Mwana
wa Mungu.
2 [b]Kama ilivyoandikwa katika kitabu cha
nabii Isaya:

"Tazama, nitamtuma mjumbe wangu
mbele yako,
atakayetengeneza njia mbele
yako":
3 [c]"sauti ya mtu aliaye nyikani.
'Itengenezeni njia ya Bwana,
yanyoosheni mapito yake.' "

4 [d]Yohana alikuja, akibatiza huko
nyikani, akihubiri ubatizo wa toba kwa
ajili ya msamaha wa dhambi. 5 [e]Watu
kutoka Uyahudi wote na sehemu zote za
Yerusalemu walikuwa wakimwendea. Nao
wakaziungama dhambi zao, akawabatiza
katika Mto Yordani. 6 [f]Yohana alivaa mavazi
yaliyotengenezwa kwa singa za ngamia na
mkanda wa ngozi kiunoni mwake. Chakula
chake kilikuwa nzige na asali ya mwitu.
7 [g]Naye alihubiri akisema, "Baada yangu
atakuja yeye aliye na uwezo kuniliko mimi,
ambaye sistahili hata kuinama na kulegeza
kamba za viatu vyake. 8 [h]Mimi nawabatiza
kwa maji, lakini yeye atawabatiza kwa
Roho Mtakatifu."

*Ubatizo Wa Yesu*

**(Mathayo 3:13-17; Luka 3:21-22)**

9 [i]Wakati huo Yesu akaja kutoka Nazareti
ya Galilaya, naye akabatizwa na Yohana
katika Mto Yordani. 10 [j]Yesu alipokuwa
akitoka ndani ya maji, aliona mbingu
zikifunguka na Roho akishuka juu yake
kama hua. 11 [k]Nayo sauti kutoka mbinguni
ikasema, "Wewe ni Mwanangu mpendwa;
nami nimependezwa nawe sana."

*Majaribu Ya Yesu*

**(Mathayo 4:1-11; Luka 4:1-13)**

12 [l]Wakati huo huo, Roho akamwongoza
Yesu kwenda nyikani, 13 [m]naye akawa
huko nyikani kwa muda wa siku arobaini,
akijaribiwa na Shetani. Alikaa na wanyama
wa mwituni, nao malaika wakamhudumia.

*Yesu Aanza Kuhubiri*

14 [n]Baada ya Yohana kukamatwa na
kutiwa gerezani, Yesu aliingia Galilaya
akaanza kuhubiri habari njema ya Mungu,
15 [o]akisema, "Wakati umewadia, Ufalme wa
Mungu umekaribia. Tubuni na kuiamini
Habari Njema."

*Yesu Awaita Wanafunzi Wanne*

**(Mathayo 4:12-22; Luka 4:14-15; 5:1-11)**

16 [p]Yesu alipokuwa akitembea kando ya
Bahari ya Galilaya, aliwaona Simoni na
Andrea nduguye wakizitupa nyavu zao
baharini, kwa kuwa wao walikuwa wavuvi.
17 [q]Yesu akawaambia, "Njooni, nifuateni
nami nitawafanya mwe wavuvi wa watu."
18 [r]Mara wakaacha nyavu zao, wakamfuata.
19 [s]Alipokwenda mbele kidogo, akamwona
Yakobo mwana wa Zebedayo na Yohana
nduguye, wakiwa kwenye mashua yao

[a]**1:1** Mt 4:3
[b]**1:2** Mal 3:1; Lk 7:27
[c]**1:3** Isa 40:3; Yn 1:23
[d]**1:4** Yn 1:26, 33; Mt 3:1; Mdo 11:16; Lk 1:7
[e]**1:5** Mt 3:5
[f]**1:6** Law 11:22; Mt 3:4
[g]**1:7** Mdo 13:25; Yn 1:27; Mdo 13:25
[h]**1:8** Yoe 2:28; Yn 1:33
[i]**1:9** Mt 2:23; Lk 3:21
[j]**1:10** Yn 1:32
[k]**1:11** Mt 3:17; Mk 9:7; Za 2:7; Isa 42:1
[l]**1:12** Mt 4:1; Lk 4:1
[m]**1:13** Mt 4:10; Ebr 4:15
[n]**1:14** Mt 4:12; 4:23; 4:12; 4:23; Lk 4:14, 15
[o]**1:15** Rum 5:6; Gal 4:4; Mdo 20:21
[p]**1:16** Mt 4:18; Lk 5:4
[q]**1:17** Mt 13:47
[r]**1:18** Mt 19:27; Lk 5:11; Mt 4:19
[s]**1:19** Mt 4:21

wakizitengeneza nyavu zao. 20 Papo hapo
akawaita, nao wakamwacha Zebedayo baba
yao kwenye mashua pamoja na watumishi
wa kuajiriwa, nao wakamfuata Yesu.

*Yesu Amtoa Pepo Mchafu*

**(Luka 4:31-37)**

21 [a]Wakaenda mpaka Kapernaumu.
Ilipofika siku ya Sabato, mara Yesu akaingia
sinagogi, akaanza kufundisha. 22 [b]Watu
wakashangaa sana kwa mafundisho yake,
kwa maana aliwafundisha kama yeye aliye
na mamlaka, wala si kama walimu wa
sheria. 23 [c]Wakati huo huo katika sinagogi
lao palikuwa na mtu aliyekuwa amepagawa
na pepo mchafu, 24 [d]naye akapiga kelele
akisema, "Tuna nini nawe, Yesu wa
Nazareti? Je, umekuja kutuangamiza?
Ninakujua wewe ni nani. Wewe ndiwe Aliye
Mtakatifu wa Mungu!"

25 [e]Lakini Yesu akamkemea, akamwambia,
"Nyamaza kimya! Nawe umtoke!" 26 [f]Yule
pepo mchafu akamtikisatikisa huyo mtu
kwa nguvu, kisha akamtoka akipiga kelele
kwa sauti kubwa.

27 [g]Watu wote wakashangaa, hata
wakaulizana wao kwa wao, "Haya ni
mambo gani? Ni mafundisho mapya, tena
yenye mamlaka! Anaamuru hata pepo
wachafu, nao wanamtii!" 28 [h]Sifa zake
zikaanza kuenea haraka katika eneo lote
la karibu na Galilaya.

*Yesu Amponya Mama Mkwe Wa Simoni*

**(Mathayo 8:14-15; Luka 4:38-39)**

29 [i]Mara walipotoka katika sinagogi,
walikwenda pamoja na Yakobo na
Yohana hadi nyumbani kwa Simoni
na Andrea. 30 Mama mkwe wa Simoni
alikuwa kitandani, ana homa, nao
wakamweleza Yesu habari zake. 31 [j]Hivyo
Yesu akamwendea, akamshika mkono na
kumwinua. Kisha homa ikamwacha, naye
akaanza kuwahudumia.

*Yesu Aponya Wengi*

**(Mathayo 8:16-17; Luka 4:40-41)**

32 [k]Jioni ile baada ya jua kutua, watu
wakamletea Yesu wagonjwa wote na
waliopagawa na pepo wachafu. 33 Mji
wote ukakusanyika mbele ya nyumba hiyo.
34 [l]Yesu akawaponya watu wengi waliokuwa
na magonjwa ya aina mbalimbali. Akawatoa
pepo wachafu wengi, lakini hakuwaacha
hao pepo wachafu waseme, kwa sababu
walimjua yeye ni nani.

*Yesu Aenda Galilaya*

**(Luka 4:42-44)**

35 [m]Alfajiri na mapema sana kulipokuwa
bado kuna giza, Yesu akaamka, akaondoka,
akaenda mahali pa faragha ili kuomba.
36 [n]Simoni na wenzake wakaenda kumtafuta,
37 nao walipomwona, wakamwambia, "Kila
mtu anakutafuta!"

38 [o]Yesu akawajibu, "Twendeni mahali
pengine kwenye vijiji jirani, ili niweze
kuhubiri huko pia, kwa sababu hicho
ndicho nilichokuja kukifanya." 39 [p]Kwa hiyo
akazunguka Galilaya kote, akihubiri katika
masinagogi yao na kutoa pepo wachafu.

*Yesu Amtakasa Mwenye Ukoma*

**(Mathayo 8:1-4; Luka 5:12-16)**

40 [q]Mtu mmoja mwenye ukoma alimjia
Yesu, akamwomba akipiga magoti,
akamwambia, "Ukitaka, waweza
kunitakasa."

41 Yesu, akiwa amejawa na huruma,
akanyoosha mkono wake akamgusa,
akamwambia, "Nataka. Takasika!" 42 Mara
ukoma ukamtoka, naye akatakasika.

[a]**1:21** Mk 1:39; Mt 4:23
[b]**1:22** Mt 7:28-29
[c]**1:23** Lk 4:33
[d]**1:24** Mt 8:29; Yn 1:45-46; Mdo 4:10; Za 16:10; 1Yn 2:20
[e]**1:25** Mk 1:34
[f]**1:26** Mk 9:20
[g]**1:27** Mk 10:24, 32
[h]**1:28** Mk 9:26
[i]**1:29** Mt 8:14; Lk 4:38
[j]**1:31** Lk 7:14
[k]**1:32** Mt 4:24
[l]**1:34** Mt 4:23; Mk 3:12; Mdo 16:17-18
[m]**1:35** Lk 3:21
[n]**1:36** Lk 4:43-44
[o]**1:38** Isa 61:1
[p]**1:39** Mt 4:23-24
[q]**1:40** Mk 10:17

43 [a]Baada ya Yesu kumwonya vikali, akamruhusu aende zake 44 [b]akimwambia, “Hakikisha humwambii mtu yeyote habari hizi, bali nenda ukajionyeshe kwa kuhani, na ukatoe sadaka alizoagiza Mose kwa utakaso wako, ili kuwa ushuhuda kwao.” 45 [c]Lakini yule mtu akaenda akaanza kutangaza habari za kuponywa kwake waziwazi. Kwa hiyo, Yesu hakuweza tena kuingia katika miji waziwazi lakini alikaa sehemu zisizo na watu. Hata hivyo watu wakamfuata huko kutoka kila upande.

### *Yesu Amponya Mtu Aliyepooza*

**(Mathayo 9:1-8; Luka 5:17-26)**

2 [d]Baada ya siku kadhaa Yesu alirudi Kapernaumu, watu wakasikia kwamba amerudi nyumbani. 2 [e]Hivyo watu wengi wakakusanyika kiasi kwamba hapakubaki nafasi yoyote hata mlangoni! Naye akawahubiria Neno. 3 [f]Ndipo baadhi ya watu wakaja wakamletea Yesu mtu aliyepooza, akiwa amebebwa na watu wanne. 4 Kwa kuwa walikuwa hawawezi kumfikisha kwa Yesu kwa ajili ya umati wa watu, walitoboa tundu kwenye paa mahali pale alipokuwa Yesu, wakamshusha yule aliyepooza kwa kitanda alichokuwa amelalia. 5 [g]Yesu alipoiona imani yao, alimwambia yule mtu aliyepooza, “Mwanangu, dhambi zako zimesamehewa.”

6 Basi baadhi ya walimu wa sheria waliokuwa wameketi huko wakawaza mioyoni mwao, 7 [h]“Kwa nini mtu huyu anasema hivi? Huyu anakufuru! Ni nani awezaye kusamehe dhambi isipokuwa Mungu peke yake?”

8 [i]Mara moja Yesu akatambua rohoni mwake kile walichokuwa wanawaza mioyoni mwao, naye akawaambia, “Kwa nini mnawaza hivyo mioyoni mwenu? 9 Je, ni lipi lililo rahisi zaidi: kumwambia huyu aliyepooza, ‘Umesamehewa dhambi zako,’ au kusema, ‘Inuka, uchukue mkeka wako, uende’? 10 [j]Lakini ili mpate kujua ya kwamba Mwana wa Adamu anayo mamlaka duniani kusamehe dhambi…” Yesu akamwambia yule aliyepooza, 11 “Nakuambia, inuka, chukua mkeka wako, uende nyumbani kwako.” 12 [k]Yule mtu aliyekuwa amepooza akasimama, akachukua mkeka wake, akatembea machoni pao wote! Jambo hili likawashangaza wote, wakamtukuza Mungu, wakisema, “Hatujapata kuona jambo kama hili kamwe!”

### *Yesu Amwita Lawi*

**(Mathayo 9:9-13; Luka 5:27-32)**

13 [l]Yesu akaenda tena kandokando ya Bahari ya Galilaya. Umati mkubwa wa watu ukamfuata, naye akaanza kuwafundisha. 14 [m]Alipokuwa akitembea, akamwona Lawi mwana wa Alfayo ameketi forodhani mahali pa kutoza ushuru, akamwambia, “Nifuate.” Lawi akaondoka, akamfuata Yesu.

15 [n]Yesu alipokuwa akila chakula nyumbani mwa Lawi, watoza ushuru wengi pamoja na “wenye dhambi” walikuwa wakila pamoja naye na wanafunzi wake, kwa maana kulikuwa na watu wengi waliokuwa wakimfuata. 16 [o]Baadhi ya walimu wa sheria waliokuwa Mafarisayo walipomwona akila pamoja na watoza ushuru na “wenye dhambi,” wakawauliza wanafunzi wake: “Mbona Yesu anakula pamoja na watoza ushuru na ‘wenye dhambi’?”

17 [p]Yesu aliposikia haya akawaambia, “Watu wenye afya hawahitaji tabibu, bali walio wagonjwa. Sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi.”

---

[a]**1:43** Mk 3:12; 7:36
[b]**1:44** Mt 8:4; Law 13:49; 14:1-32
[c]**1:45** Lk 5:15-16, 17; Yn 6:2
[d]**2:1** Mt 9:4
[e]**2:2** Mk 1:45; 2:13
[f]**2:3** Mt 4:24
[g]**2:5** Lk 7:48
[h]**2:7** Isa 43:25
[i]**2:8** Mt 9:4
[j]**2:10** Mt 8:20
[k]**2:12** Mt 9:8; 9:33
[l]**2:13** Lk 5:15; Yn 6:2
[m]**2:14** Mt 4:19
[n]**2:15** Mt 9:10
[o]**2:16** Mdo 23:9; 9:11
[p]**2:17** Lk 19:10; 1Tim 1:15

*Yesu Aulizwa Kuhusu Kufunga*

**(Mathayo 9:14-17; Luka 5:33-39)**

18 [a]Basi wanafunzi wa Yohana pamoja na
Mafarisayo walikuwa wakifunga. Baadhi
ya watu wakamjia Yesu na kumuuliza,
“Mbona wanafunzi wa Yohana na wa
Mafarisayo hufunga lakini wanafunzi wako
hawafungi?”
19 Yesu akawajibu, “Wageni wa bwana
arusi wawezaje kufunga wakati angali
pamoja nao? Wakati bwana arusi bado
yuko pamoja nao, hawawezi kufunga.
20 [b]Lakini wakati utafika ambapo bwana
arusi ataondolewa kwao. Siku hiyo ndipo
watakapofunga.
21 “Hakuna mtu ashoneaye kiraka cha
nguo mpya kwenye nguo iliyochakaa.
Akifanya hivyo, kile kiraka kipya
kitachanika kutoka ile nguo iliyochakaa,
nayo itachanika zaidi. 22 [c]Wala hakuna
mtu awekaye divai mpya kwenye viriba
vikuukuu. Akifanya hivyo, ile divai mpya
itavipasua hivyo viriba, nayo hiyo divai
itamwagika na viriba vitaharibika. Lakini
divai mpya huwekwa kwenye viriba vipya.”

*Bwana Wa Sabato*

**(Mathayo 12:1-8; Luka 6:1-5)**

23 [d]Siku moja ya Sabato, Yesu pamoja
na wanafunzi wake walikuwa wakipita
katikati ya mashamba ya nafaka.
Walipokuwa wakitembea, wanafunzi wake
wakaanza kuvunja masuke. 24 [e]Mafarisayo
wakamwambia, “Tazama, mbona
wanafanya jambo lisilo halali kufanywa
siku ya Sabato?”
25 Yesu akawajibu, “Je, hamjasoma
kamwe alivyofanya Daudi wakati yeye
na wenzake walikuwa na njaa, wakahitaji
chakula? 26 [f]Daudi aliingia katika nyumba
ya Mungu, wakati Abiathari alikuwa kuhani
mkuu, akaila ile mikate iliyowekwa wakfu,
ambayo ni halali kuliwa na makuhani peke
yao. Naye pia akawapa wenzake.”
27 [g]Kisha Yesu akawaambia, “Sabato
ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu,
lakini si mwanadamu kwa ajili ya Sabato.
28 [h]Hivyo, Mwana wa Adamu ndiye Bwana
wa Sabato.”

*Mtu Aliyepooza Mkono Aponywa*

**(Mathayo 12:9-14; Luka 6:6-11)**

3 [i]Yesu akaingia tena ndani ya sinagogi,
na huko palikuwa na mtu aliyepooza
mkono. 2 [j]Wakawa wanamwangalia waone
kama atamponya siku ya Sabato, ili wapate
sababu ya kumshtaki. 3 Yesu akamwambia
yule mwenye mkono uliopooza, “Njoo hapa
mbele ya watu wote.”
4 Kisha Yesu akawauliza, “Je, ni lipi lililo
halali siku ya Sabato: Ni kutenda mema
au kutenda mabaya? Ni kuokoa maisha au
kuua?” Lakini wao wakanyamaza kimya.
5 [k]Yesu akawatazama pande zote kwa
hasira, akahuzunika sana kwa ajili ya
ugumu wa mioyo yao. Akamwambia
yule mtu mwenye mkono uliopooza,
“Nyoosha mkono wako.” Akaunyoosha,
nao ukaponywa kabisa! 6 [l]Kisha Mafarisayo
wakatoka nje, nao wakaanza kufanya shauri
la kumuua Yesu wakiwa na Maherode.

*Umati Wa Watu Wamfuata Yesu*

7 [m]Yesu pamoja na wanafunzi wake
wakaondoka huko wakaenda baharini, nao
umati mkubwa wa watu kutoka Galilaya
ukamfuata. 8 [n]Waliposikia mambo yote
aliyokuwa akiyafanya, umati mkubwa wa
watu ukamjia kutoka Uyahudi, Yerusalemu,
Idumaya, na ng’ambo ya Yordani, pamoja
na wale wa sehemu za karibu na Tiro na
Sidoni. 9 Kwa sababu ya umati mkubwa
wa watu, aliwaambia wanafunzi wake
waweke tayari mashua ndogo kwa ajili

---

[a]**2:18** Mt 6:16-18; Mdo 1; Mt 9
[b]**2:20** Lk 17:22
[c]**2:22** Lk 5:33-38
[d]**2:23** Kum 23:25; Mt 12:1; Lk 6:1
[e]**2:24** Mt 12:2
[f]**2:26** 1Nya 24:6; 2Sam 8:17; Law 24:5-9; 1Sam 21:1-6
[g]**2:27** Kut 23:12; Kum 5:14; Kol 2:16
[h]**2:28** Mt 8:20
[i]**3:1** Mt 4:23; Mk 1:21
[j]**3:2** Mt 12:10; Lk 14:1
[k]**3:5** Yn 11:33
[l]**3:6** Mt 22:16; Mk 12:13; Mt 12:14
[m]**3:7** Mt 4:25
[n]**3:8** Mt 11:21

yake, ili kuwazuia watu kumsonga. 10 [a]Kwa
kuwa alikuwa amewaponya wagonjwa
wengi, wale wenye magonjwa walikuwa
wanasukumana ili wapate kumgusa.
11 [b]Kila mara pepo wachafu walipomwona,
walianguka chini mbele yake na kupiga
kelele wakisema, “Wewe ndiwe Mwana wa
Mungu.” 12 [c]Lakini aliwaonya wasimseme
yeye ni nani.

*Yesu Achagua Mitume Kumi Na Wawili*

**(Mathayo 10:1-4; Luka 6:12-16)**

13 [d]Yesu akapanda mlimani na kuwaita
wale aliowataka, nao wakamjia.
14 [e]Akawachagua kumi na wawili, ambao
aliwaita mitume, ili wapate kuwa pamoja
naye, na awatume kwenda kuhubiri 15 [f]na
kuwa na mamlaka ya kutoa pepo wachafu.
16 [g]Hawa ndio wale kumi na wawili
aliowachagua: Simoni (ambaye alimwita
Petro); 17 [h]Yakobo mwana wa Zebedayo, na
Yohana nduguye (ambao aliwaita Boanerge,
maana yake Wana wa Ngurumo); 18 Andrea,
Filipo, Bartholomayo, Mathayo, Tomaso,
Yakobo mwana wa Alfayo, Thadayo,
Simoni Mkananayo, 19 na Yuda Iskariote
aliyemsaliti Yesu.

*Yesu Na Beelzebuli*

**(Mathayo 12:22-32; Luka 11:14-23; 12:10)**

20 [i]Kisha Yesu aliporudi nyumbani, umati
wa watu ukakusanyika tena, kiasi kwamba
yeye na wanafunzi wake hawakuweza kula
chakula. 21 [j]Ndugu zake walipopata habari
wakaja ili kumchukua kwa maana watu
walikuwa wakisema, “Amerukwa na akili.”
22 [k]Walimu wa sheria walioteremka
kutoka Yerusalemu walisema, “Amepagawa
na Beelzebuli![l] Anatoa pepo wachafu kwa
kutumia mkuu wa pepo wachafu!”
23 [m]Basi Yesu akawaita na kuzungumza
nao kwa mifano akasema: “Shetani
awezaje kumtoa Shetani? 24 Kama ufalme
ukigawanyika dhidi yake wenyewe, ufalme
huo hauwezi kusimama. 25 Nayo nyumba
kama ikigawanyika dhidi yake yenyewe,
nyumba hiyo haiwezi kusimama. 26 Naye
Shetani kama akijipinga mwenyewe na
awe amegawanyika, hawezi kusimama
bali mwisho wake umewadia. 27 [n]Hakuna
mtu yeyote awezaye kuingia kwenye
nyumba ya mtu mwenye nguvu na kuteka
nyara mali zake asipomfunga kwanza yule
mwenye nguvu. Ndipo ataweza kuteka
nyara mali zake. 28 [o]Amin, nawaambia,
dhambi zote na makufuru yote ya
wanadamu watasamehewa. 29 [p]Lakini
yeyote anayemkufuru Roho Mtakatifu
hatasamehewa kamwe, atakuwa na hatia
ya dhambi ya milele.”
30 [q]Yesu alisema hivi kwa sababu
walikuwa wanasema, “Ana pepo mchafu.”

*Mama Na Ndugu Zake Yesu*

**(Mathayo 12:46-50; Luka 8:19-21)**

31 [r]Kisha wakaja ndugu zake Yesu
pamoja na mama yake. Wakasimama nje,
wakamtuma mtu kumwita. 32 Umati wa
watu ulikuwa umeketi kumzunguka, nao
wakamwambia, “Mama yako na ndugu zako
wako nje, wanakutafuta.”
33 Akawauliza, “Mama yangu na ndugu
zangu ni nani?”
34 Kisha akawatazama wale watu
waliokuwa wameketi kumzunguka pande
zote, akasema, “Hawa ndio mama yangu
na ndugu zangu. 35 Mtu yeyote anayetenda
mapenzi ya Mungu, huyo ndiye ndugu
yangu, na dada yangu na mama yangu.”

---

[a]**3:10** Mt 4:23; 9:20
[b]**3:11** Mt 4:3; Mk 1:23, 24
[c]**3:12** Mt 8:4; Mdo 16:17, 18
[d]**3:13** Mt 5:11
[e]**3:14** Mk 6:30
[f]**3:15** Mt 10:1
[g]**3:16** Yn 1:42
[h]**3:17** Lk 2
[i]**3:20** Mk 6:31
[j]**3:21** Yn 10:20; Mdo 26:24
[k]**3:22** Mt 15:1; 12:24; Yn 10:20; Mt 9:34
[l]22 Beelzebuli kwa Kiyunani ni Beelzebubu, yaani mkuu wa pepo wachafu.
[m]**3:23** Mk 4:2; Mt 4:10
[n]**3:27** Isa 49:24-25
[o]**3:28** Mt 12:31; Lk 12:10; 1Yn 5:16
[p]**3:29** Mt 12:31-32; Lk 12:10
[q]**3:30** Mk 3:22
[r]**3:31** Mt 12:46; Lk 8:19

### *Mfano Wa Mpanzi*

**(Mathayo 13:1-9; Luka 8:4-8)**

4 [a]Yesu akaanza kufundisha tena kando
ya bahari. Umati wa watu uliokuwa
umekusanyika kumzunguka ulikuwa
mkubwa, kiasi kwamba ilimbidi Yesu
aingie kwenye mashua iliyokuwa baharini
na kuketi humo, nao watu wote walikuwa
ufuoni mwa bahari. 2 [b]Akawafundisha
mambo mengi kwa mifano, naye katika
mafundisho yake akasema: 3 [c]“Sikilizeni!
Mpanzi alitoka kwenda kupanda mbegu
zake. 4 Alipokuwa akitawanya mbegu,
nyingine zilianguka kando ya njia, nao
ndege wakaja na kuzila. 5 Nyingine
zilianguka kwenye ardhi yenye mwamba
isiyo na udongo wa kutosha. Zikaota haraka,
kwa kuwa udongo ulikuwa haba. 6 Lakini
jua lilipozidi, mimea ikanyauka na kukauka
kwa kuwa mizizi yake haikuwa na kina.
7 Mbegu nyingine zilianguka kwenye miiba,
nayo miiba hiyo ikakua, ikaisonga hiyo
mimea, hivyo haikutoa mazao. 8 [d]Mbegu
nyingine zilianguka kwenye udongo mzuri,
zikaota vizuri na kukua, zikatoa mazao,
moja mara thelathini, nyingine mara sitini,
na nyingine mara mia moja.”
9 [e]Kisha Yesu akasema, “Mwenye masikio
ya kusikia, na asikie.”

### *Sababu Za Mifano*

**(Mathayo 13:10-17; Luka 8:9-10)**

10 [f]Alipokuwa peke yake, watu
waliokuwepo naye pamoja na wanafunzi
wake kumi na wawili wakamuuliza kuhusu
mifano yake. 11 [g]Naye akawaambia, “Ninyi
mmepewa kujua siri ya Ufalme wa Mungu.
Lakini kwa wale walioko nje, kila kitu
husemwa kwao kwa mifano, 12 [h]ili,

“ ‘daima waone lakini wasitambue,
daima wasikie lakini wasielewe;
wasije wakageuka, wakatubu na
kusamehewa!’ ”

### *Yesu Afafanua Maana Ya Mfano Wa Mbegu*

**(Mathayo 13:18-23; Luka 8:11-15)**

13 Kisha Yesu akawauliza, “Hamwelewi
maana ya mfano huu? Basi mtaelewaje
mifano mingine? 14 [i]Yule mpanzi hupanda
neno. 15 [j]Hawa ndio wale walio kando ya
njia ambako neno lilipandwa. Walisikiapo
neno, Shetani huja mara na kulinyakua
lile neno lililopandwa ndani yao. 16 Nazo
zile mbegu zilizoanguka kwenye udongo
wenye miamba, ni wale wanaolisikia neno,
na mara hulipokea kwa furaha. 17 Lakini
kwa kuwa hawana mizizi, wao hudumu
kwa muda mfupi tu. Kisha dhiki au mateso
yanapoinuka kwa ajili ya lile neno, mara
wao huiacha imani. 18 Lakini wengine, kama
mbegu iliyopandwa kwenye miiba, hulisikia
lile neno; 19 [k]lakini masumbufu ya maisha
haya, na udanganyifu wa mali na tamaa
ya mambo mengine huja na kulisonga lile
neno na kulifanya lisizae. 20 Wengine, kama
mbegu iliyopandwa kwenye udongo mzuri,
hulisikia lile neno, wakalipokea na kuzaa
mazao. Wao huzaa mara thelathini, au mara
sitini, au mara mia ya mbegu iliyopandwa.”

### *Mfano Wa Taa*

**(Luka 8:16-18)**

21 [l]Akawaambia, “Je, taa huwashwa na
kufunikwa chini ya kikapu au mvunguni
mwa kitanda? Je, haiwashwi na kuwekwa
juu ya kinara chake? 22 [m]Kwa kuwa hakuna
kilichofichika ambacho hakitafunuliwa,
wala hakuna jambo lolote la siri ambalo
halitaletwa nuruni. 23 [n]Mwenye masikio ya
kusikia, na asikie.”
24 [o]Naye akawaambia, “Kuweni
waangalifu na yale mnayosikia. Kipimo
kile mpimacho, ndicho mtakachopimiwa

---

[a]**4:1** Mk 2:13; 3:7
[b]**4:2** Mk 2:11; 3:23
[c]**4:3** Mk 4:26
[d]**4:8** Yn 15:5; Kol 1:16
[e]**4:9** Mk 4:23; Mt 11:15
[f]**4:10** Mt 13:10; Lk 8:9
[g]**4:11** Mt 3:2; 1The 4:12; 1Tim 3:7
[h]**4:12** Isa 6:9-10; Mk 13:13-15
[i]**4:14** Mdo 16:6; Flp 1:14
[j]**4:15** Mt 4:10
[k]**4:19** 1Tim 6:9-17; 1Yn 2:15-17
[l]**4:21** Mt 5:15
[m]**4:22** Yer 16:17; Lk 12:2
[n]**4:23** Mk 4:9; Mt 11:15
[o]**4:24** Mt 7:2; Lk 6:38

ninyi, hata na zaidi. [25] [a]Kwa maana kila mtu aliye na kitu atapewa zaidi, naye atakuwa navyo tele. Lakini yule asiye na kitu, hata kile alicho nacho atanyang'anywa."

*Mfano Wa Mbegu Inayoota*

[26] [b]Pia akawaambia, "Ufalme wa Mungu unafanana na mtu apandaye mbegu
shambani. [27] [c]Akiisha kuzipanda, usiku na mchana, akiwa amelala au ameamka, mbegu huota na kukua pasipo yeye kujua
ikuavyo. [28] Udongo huifanya iote kuwa mche, halafu suke, kisha nafaka kamili
kwenye suke. [29] [d]Lakini nafaka inapokuwa imekomaa, mara mkulima huingia shambani na mundu wa kuvunia, maana mavuno yamekuwa tayari."

*Mfano Wa Mbegu Ya Haradali*

**(Mathayo 13:31-32, 34; Luka 13:18-19)**

[30] [e]Akawaambia tena, "Tuufananishe Ufalme wa Mungu na nini? Au tutumie
mfano gani ili kuueleza? [31] Ni kama punje ya haradali, ambayo ni mbegu ndogo sana kuliko mbegu zote zinazopandwa ardhini.
[32] [f]Lakini ikishaota, hukua ikawa mmea mkubwa kuliko yote ya bustanini, ikawa na matawi makubwa hata ndege wa angani wanaweza kujenga viota kwenye matawi yake."

[33] [g]Kwa mifano mingine mingi kama hii Yesu alinena nao neno lake, kwa kadiri
walivyoweza kulielewa. [34] [h]Hakusema nao neno lolote pasipo mfano. Lakini alipokuwa na wanafunzi wake, aliwafafanulia kila kitu.

*Yesu Atuliza Dhoruba*

**(Mathayo 8:23-27; Luka 8:22-25)**

[35] [i]Siku hiyo ilipokaribia jioni, aliwaambia wanafunzi wake, "Tuvukeni
twende mpaka ng'ambo." [36] [j]Wakauacha ule umati wa watu, na wakamchukua vile alivyokuwa kwenye mashua. Palikuwa pia na mashua nyingine nyingi pamoja naye.
[37] Kukawa na dhoruba kali, nayo mawimbi yakaipiga ile mashua hata ikawa karibu
kujaa maji. [38] Yesu alikuwa katika shetri, akiwa analala juu ya mto. Wanafunzi wake wakamwamsha, wakamwambia, "Mwalimu, hujali kama tunazama?"

[39] Akaamka, akaukemea ule upepo, akayaambia yale mawimbi, "Uwe kimya! Tulia!" Ule upepo ukatulia, kukawa shwari kabisa.

[40] [k]Yesu akawaambia wanafunzi wake, "Kwa nini mnaogopa hivyo? Je, bado hamna imani?"

[41] Nao wakawa wameogopa sana, wakaulizana, "Ni nani huyu ambaye hata upepo na mawimbi vinamtii?"

*Yesu Amponya Mtu Mwenye Pepo*

**(Mathayo 8:28-34; Luka 8:26-39)**

5 [l]Wakafika upande wa pili wa ziwa wakaingia katika nchi ya Wagerasi.
[2] [m]Yesu alipotoka kwenye mashua, mara mtu mmoja mwenye pepo mchafu akatoka
makaburini akakutana naye. [3] Mtu huyu aliishi makaburini, wala hakuna aliyeweza kumzuia hata kwa kumfunga minyororo.
[4] Kwa kuwa mara kwa mara alikuwa amefungwa minyororo mikononi na miguuni, lakini akaikata hiyo minyororo na kuzivunja zile pingu miguuni mwake. Hapakuwa na mtu yeyote aliyekuwa na
nguvu za kumzuia. [5] Usiku na mchana alikuwa makaburini na milimani, akipiga kelele na kujikatakata kwa mawe.

[6] Alipomwona Yesu kwa mbali, alimkimbilia, akapiga magoti mbele yake.
[7] [n]Akapiga kelele kwa nguvu akisema, "Una nini nami, Yesu, Mwana wa Mungu Aliye Juu Sana? Ninakusihi kwa jina la Mungu,
usinitese!" [8] Kwa kuwa Yesu alikuwa

[a]**4:25** Mt 13:12; 25:29
[b]**4:26** Mt 13:24
[c]**4:27** Yak 5:7
[d]**4:29** Ufu 14:15; Yoe 3:13
[e]**4:30** Mt 13:24
[f]**4:32** Dan 4:12, 21; Eze 17:23; 31; 6
[g]**4:33** Yn 16:25; Mt 13:34
[h]**4:34** Yn 16:25
[i]**4:35** Mt 8:18, 23-27; Lk 8:22-25
[j]**4:36** Mk 5:2, 21; 6:32, 45
[k]**4:40** Mt 14:31
[l]**5:1** Mt 8:28; Mk 8:26
[m]**5:2** Mk 4:1; 1:23
[n]**5:7** Mt 8:29; Mdo 16:17; Ebr 7:1

amemwambia, “Mtoke mtu huyu, wewe
pepo mchafu!”
9 Yesu akamuuliza, “Jina lako ni nani?”
Akamjibu, “Jina langu ni Legioni,[a] kwa
kuwa tuko wengi.” 10 Akamsihi Yesu sana
asiwapeleke nje ya nchi ile.
11 Palikuwa na kundi kubwa la nguruwe
lililokuwa likilisha karibu kando ya kilima.
12 Wale pepo wachafu wakamsihi Yesu
wakisema, “Tuamuru twende kwenye wale
nguruwe. Turuhusu tuwaingie.” 13 Basi Yesu
akawaruhusu, nao wale pepo wachafu
wakatoka, wakawaingia hao nguruwe. Lile
kundi lilikuwa na nguruwe wapatao 2,000,
nao wote wakateremkia gengeni kwa kasi,
nao wakatumbukia ziwani na kuzama.
14 Wale watu waliokuwa wakichunga
hao nguruwe wakakimbilia mjini na
vijijini kueleza yaliyotukia. Watu wakatoka
kwenda kuona hayo yaliyokuwa yametukia.
15 [b]Walipofika kwa Yesu, wakamwona yule
mtu aliyekuwa amepagawa na pepo wachafu
legioni akiwa ameketi hapo, amevaa nguo na
mwenye akili timamu. Wakaogopa. 16 Wale
walioyaona mambo hayo wakawaeleza
watu wengine yaliyomtokea yule mtu
aliyekuwa amepagawa na pepo wachafu, na
habari za lile kundi la nguruwe pia. 17 [c]Basi
watu wakaanza kumwomba Yesu aondoke
katika nchi yao.
18 [d]Yesu alipokuwa anaingia kwenye
mashua, yule mtu aliyekuwa amepagawa
na pepo wachafu akamsihi Yesu
waende pamoja. 19 [e]Yesu hakumruhusu,
bali alimwambia, “Nenda nyumbani
kwa jamaa yako ukawaeleze mambo
makuu aliyokutendea Bwana, na jinsi
alivyokuhurumia.” 20 [f]Yule mtu akaenda
zake, akaanza kutangaza katika Dekapoli
mambo makuu Yesu aliyomtendea. Nao
watu wote wakastaajabu.

*Mwanamke Aponywa*

**(Mathayo 9:18-26; Luka 8:40-56)**

21 [g]Yesu alipokwisha kuvuka tena na
kufika ng’ambo, umati mkubwa wa watu
ukamzunguka yeye akiwa hapo kando ya
bahari. 22 [h]Kisha mmoja wa viongozi wa
sinagogi aliyeitwa Yairo akafika pale. Naye
alipomwona Yesu, akapiga magoti miguuni
pake, 23 [i]akamsihi akisema, “Binti yangu
mdogo ni mgonjwa mahututi. Tafadhali
nakusihi, njoo uweke mikono yako juu
yake ili apate kupona, naye atakuwa hai.”
24 Hivyo Yesu akaenda pamoja naye.
Umati mkubwa wa watu ukamfuata,
nao watu wakawa wanamsonga. 25 [j]Hapo
palikuwa na mwanamke aliyekuwa
amesumbuliwa na tatizo la kutokwa damu
kwa miaka kumi na miwili. 26 Mwanamke
huyu alikuwa ameteseka sana kwa mikono
ya matabibu wengi, na kutumia kila kitu
alichokuwa nacho. Lakini badala ya kupona,
hali yake ilizidi kuwa mbaya. 27 Alikuwa
amesikia habari za Yesu, naye akaja kwa
nyuma yake kwenye umati wa watu,
akaligusa vazi lake, 28 [k]kwa maana alisema
moyoni mwake, “Kama nikiweza kuligusa
vazi lake tu, nitaponywa.” 29 [l]Mara kutoka
damu kwake kukakoma, naye akajisikia
mwilini mwake amepona kabisa.
30 [m]Ghafula Yesu akatambua kuwa nguvu
zimemtoka. Akaugeukia ule umati wa watu
na kuuliza, “Ni nani aliyegusa mavazi
yangu?”
31 Wanafunzi wake wakamjibu, “Unaona
jinsi umati wa watu unavyokusonga.
Wawezaje kuuliza, ‘Ni nani aliyenigusa?’ ”
32 Lakini Yesu akaangalia pande zote
ili aone ni nani aliyemgusa. 33 Yule
mwanamke, akijua kilichomtokea, akaja,
akaanguka miguuni pake akitetemeka
kwa hofu, akamweleza ukweli wote.
34 [n]Yesu akamwambia, “Binti, imani yako

[a]9 Legioni maana yake ni Jeshi.
[b]**5:15** Mk 5:9; 5:18-19; 4:24
[c]**5:17** Mt 8:34; Mdo 16:39
[d]**5:18** Lk 8:38
[e]**5:19** Mt 8:4
[f]**5:20** Mt 4:25; Mk 7:31
[g]**5:21** Mt 9:1; Mk 4:1
[h]**5:22** Lk 13:14; Mdo 13:15
[i]**5:23** Mt 19:13
[j]**5:25** Law 15:25-30
[k]**5:28** Mt 5:20
[l]**5:29** Mk 5:34
[m]**5:30** Lk 5:17; 6:19
[n]**5:34** Mt 9:22; Mdo 15:33

imekuponya. Nenda kwa amani, upone kabisa ugonjwa wako."

### *Yesu Amfufua Binti Yairo*

35 [a]Alipokuwa bado anaongea, watu wakafika kutoka nyumbani kwa Yairo. Wakamwambia, "Binti yako amekufa. Kwa nini kuendelea kumsumbua Mwalimu?"

36 Aliposikia hayo waliyosema, Yesu akamwambia huyo kiongozi wa sinagogi, "Usiogope. Amini tu."

37 [b]Hakumruhusu mtu mwingine yeyote amfuate isipokuwa Petro, Yakobo na Yohana, nduguye Yakobo. 38 [c]Walipofika nyumbani kwa yule kiongozi wa sinagogi, Yesu akaona ghasia, watu wakilia na kuomboleza kwa sauti kubwa. 39 [d]Alipokwisha kuingia ndani, akawaambia, "Kwa nini mnafanya ghasia na kulia? Mtoto hajafa, bali amelala tu." 40 [e]Wale watu wakamcheka kwa dharau.

Lakini yeye akawatoa wote nje, akawachukua baba na mama wa yule mtoto, pamoja na wale wanafunzi aliokuwa nao. Wakaingia ndani mpaka pale alipokuwa yule mtoto. 41 [f]Akamshika mtoto mkono, akamwambia, *"Talitha koum!"* [g] (maana yake ni, "Msichana, nakuambia: amka!") 42 Mara yule msichana akasimama, akaanza kutembea (alikuwa na umri wa miaka kumi na miwili). Walipoona haya, wakastaajabu sana. 43 [h]Yesu akawaagiza kwa ukali wasimweleze mtu yeyote jambo hilo, naye akawaambia wampe yule msichana chakula.

### *Nabii Hana Heshima Kwao*

**(Mathayo 13:53-58; Luka 4:16-30)**

6 [i]Yesu akaondoka huko na kwenda mji wa kwao, akiwa amefuatana na wanafunzi wake. 2 [j]Ilipofika siku ya Sabato, akaanza kufundisha katika sinagogi, na wengi waliomsikia wakashangaa.

Nao wakauliza, "Mtu huyu ameyapata wapi mambo haya yote? Tazama ni hekima ya namna gani hii aliyopewa? Tazama matendo ya miujiza ayafanyayo kwa mikono yake! 3 [k]Huyu si yule seremala, mwana wa Maria? Na ndugu zake si Yakobo, Yose,[l] Yuda na Simoni? Dada zake wote si tuko nao hapa kwetu?" Nao wakachukizwa sana kwa ajili yake, wakakataa kumwamini.

4 [m]Yesu akawaambia, "Nabii hakosi heshima isipokuwa katika mji wake mwenyewe, na miongoni mwa jamaa na ndugu zake, na nyumbani kwake." 5 [n]Hakufanya miujiza yoyote huko isipokuwa kuweka mikono yake juu ya wagonjwa wachache na kuwaponya. 6 [o]Naye akashangazwa sana kwa jinsi wasivyokuwa na imani.

### *Yesu Awatuma Wale Kumi Na Wawili*

**(Mathayo 10:5-15; Luka 9:1-6)**

Kisha Yesu akawa anakwenda kutoka kijiji kimoja hadi kingine akifundisha. 7 [p]Akawaita wale kumi na wawili, akawatuma wawili wawili, na kuwapa mamlaka kutoa pepo wachafu.

8 Akawaagiza akisema, "Msichukue chochote kwa ajili ya safari isipokuwa fimbo tu. Msichukue mkate, wala mkoba, wala fedha kwenye mikanda yenu. 9 [q]Vaeni viatu, lakini msivae nguo ya ziada." 10 [r]Akawaambia, "Mkiingia kwenye nyumba yoyote, kaeni humo hadi mtakapoondoka katika mji huo. 11 [s]Kama mahali popote hawatawakaribisha wala kuwasikiliza, mtakapoondoka huko, kung'uteni mavumbi kutoka kwenye miguu yenu ili kuwa ushuhuda dhidi yao."

---

[a]**5:35** Mk 5:22
[b]**5:37** Mt 4:21
[c]**5:38** Mt 5:22
[d]**5:39** Mt 9:24
[e]**5:40** Mdo 9:40
[f]**5:41** Mk 1:31; Lk 7:14; Mdo 9:40
[g]41 *Talitha koum* ni lugha ya Kiaramu.
[h]**5:43** Mt 8:4
[i]**6:1** Mt 2:23; 13:54; Lk 4:16
[j]**6:2** Mk 1:21; Mt 4:23; 7:28
[k]**6:3** Mt 12:46; 11:6; Yn 6:61
[l]3 Yosefu kwa Kiyunani ni Joses.
[m]**6:4** Lk 4:24; Yn 4:44
[n]**6:5** Mk 5:23; Mwa 19; 22; 32:25; Mt 13:58
[o]**6:6** Mt 9:35; Lk 13:22
[p]**6:7** Mk 3:13; Kum 17:6; Lk 10:1; Mt 10:1
[q]**6:9** Mdo 12:8
[r]**6:10** Mt 10:11; Lk 9:4; 10:7, 8
[s]**6:11** Mt 10:14

12 [a]Kwa hiyo wakatoka na kuhubiri
kwamba inawapasa watu kutubu na kuacha
dhambi. 13 [b]Wakatoa pepo wachafu wengi,
wakawapaka wagonjwa wengi mafuta na
kuwaponya.

*Yohana Mbatizaji Akatwa Kichwa*

**(Mathayo 14:1-12; Luka 9:7-9)**

14 [c]Mfalme Herode akasikia habari
hizi, kwa maana jina la Yesu lilikuwa
limejulikana sana. Watu wengine walikuwa
wakisema, "Yohana Mbatizaji amefufuliwa
kutoka kwa wafu, ndiyo sababu nguvu
za kutenda miujiza zinafanya kazi ndani
yake."

15 [d]Wengine wakasema, "Yeye ni Eliya."

Nao wengine wakasema, "Yeye ni nabii,
kama mmojawapo wa wale manabii wa
zamani."

16 [e]Lakini Herode aliposikia habari hizi,
akasema, "Huyo ni Yohana Mbatizaji,
niliyemkata kichwa, amefufuliwa kutoka
kwa wafu!"

17 [f]Kwa kuwa Herode alikuwa ameagiza
kwamba Yohana Mbatizaji akamatwe,
afungwe na kutiwa gerezani. Alifanya hivi
kwa sababu ya Herodia, mke wa Filipo,
ndugu yake, ambaye Herode alikuwa
amemwoa. 18 [g]Yohana alikuwa amemwambia
Herode, "Si halali kwako kuwa na mke
wa ndugu yako." 19 Kwa hiyo Herodia
alikuwa amemwekea Yohana kinyongo
akataka kumuua. Lakini hakuweza, 20 [h]kwa
sababu Herode alimwogopa Yohana akijua
kwamba ni mtu mwenye haki na mtakatifu,
hivyo akamlinda. Herode alifadhaika sana
alipomsikia Yohana, lakini bado alipenda
kumsikiliza.

21 [i]Mfalme Herode alifanya karamu
kubwa wakati wa sikukuu ya kuzaliwa
kwake. Akawaalika maafisa wake wakuu,
majemadari wa jeshi na watu mashuhuri wa
Galilaya. Hatimaye Herodia alipata wasaa
aliokuwa akiutafuta. 22 Binti yake Herodia
alipoingia na kucheza, akamfurahisha
Herode pamoja na wageni wake walioalikwa
chakulani.

Mfalme Herode akamwambia yule binti,
"Niombe kitu chochote utakacho, nami
nitakupa." 23 [j]Tena akamwahidi kwa kiapo,
akamwambia, "Chochote utakachoomba
nitakupa, hata kama ni nusu ya ufalme
wangu."

24 Yule binti akatoka nje, akaenda
kumuuliza mama yake, "Niombe nini?"

Mama yake akamjibu, "Omba kichwa cha
Yohana Mbatizaji."

25 Yule binti akarudi haraka kwa mfalme,
akamwambia, "Nataka unipe sasa hivi
kichwa cha Yohana Mbatizaji kwenye
sinia."

26 [k]Mfalme akasikitika sana, lakini kwa
sababu alikuwa ameapa viapo mbele ya
wageni wake, hakutaka kumkatalia. 27 Mara
mfalme akatuma askari mmojawapo wa
walinzi wake kukileta kichwa cha Yohana.
Akaenda na kumkata Yohana kichwa humo
gerezani, 28 akakileta kichwa chake kwenye
sinia na kumpa yule msichana, naye yule
msichana akampa mama yake. 29 Wanafunzi
wa Yohana walipopata habari hizi, wakaja
na kuuchukua mwili wake, wakauzika
kaburini.

*Yesu Awalisha Wanaume 5,000*

**(Mathayo 14:13-21; Luka 9:10-17; Yohana 6:1-14)**

30 [l]Wale mitume wakakusanyika kwa
Yesu na kumpa taarifa ya mambo yote
waliyokuwa wamefanya na kufundisha.
31 [m]Basi kwa kuwa watu wengi mno
walikuwa wakija na kutoka, hata wakawa
hawana nafasi ya kula, Yesu akawaambia
wanafunzi wake, "Twendeni peke yetu
mahali pa faragha, mpate kupumzika."

32 [n]Hivyo wakaondoka kwa mashua

[a]**6:12** Lk 9:6
[b]**6:13** Yak 5:14
[c]**6:14** Mt 3:1
[d]**6:15** Mal 4:5; Mt 2:11; 16:14; Mk 8:28
[e]**6:16** Mt 14:2; Lk 3:19
[f]**6:17** Mt 11:12; Lk 3:19-20
[g]**6:18** Law 18:16; 20:21
[h]**6:20** Mt 11:9; 21:26
[i]**6:21** Es 1:3; 2:18; Lk 3:1
[j]**6:23** Es 5:3-6; 7:2
[k]**6:26** Mt 14:9
[l]**6:30** Lk 24:10; Mdo 1:2, 26; Lk 9:10
[m]**6:31** Mk 3:20
[n]**6:32** Mk 6:45; 4:36

peke yao, wakaenda mahali pasipo na watu. 33 Lakini watu wengi waliowaona wakiondoka, wakawatambua, nao wakaenda haraka kwa miguu kutoka miji yote, nao wakatangulia kufika. 34 [a]Yesu alipofika kando ya bahari, aliona makutano makubwa ya watu, akawahurumia kwa maana walikuwa kama kondoo wasiokuwa na mchungaji. Kwa hiyo akaanza kuwafundisha mambo mengi.

35 [b]Mchana ulipokuwa umeendelea sana, wanafunzi wake walienda kwake, wakamwambia, “Mahali hapa ni nyikani, nazo saa zimekwenda sana. 36 Waage watu ili waende mashambani na vijijini jirani, wakajinunulie chakula.”

37 [c]Lakini Yesu akawajibu, “Ninyi wapeni chakula.”

Wakamwambia, “Je, twende tukanunue mikate ya dinari 200[d] ili tuwape watu hawa wale?”

38 [e]Akawauliza, “Kuna mikate mingapi? Nendeni mkaangalie.”

Walipokwisha kujua wakarudi, wakamwambia, “Kuna mikate mitano na samaki wawili.”

39 Kisha Yesu akawaamuru wawaketishe watu makundi makundi kwenye majani, 40 nao wakaketi kwenye makundi ya watu mia mia na wengine hamsini hamsini. 41 [f]Yesu akaichukua ile mikate mitano na wale samaki wawili, akainua macho yake akatazama mbinguni, akavibariki na kuimega ile mikate. Kisha akawapa wanafunzi wake ili wawagawie wale watu wote. Pia akawagawia wote wale samaki wawili. 42 Watu wote wakala, wakashiba. 43 [g]Nao wanafunzi wake wakakusanya vipande vilivyosalia vya mikate na samaki, wakajaza vikapu kumi na viwili. 44 Idadi ya wanaume waliokula walikuwa 5,000.

[a]**6:34** Mt 9:36
[b]**6:35** Mk 8:1-9; Mt 14:15; Lk 9:11
[c]**6:37** 2Fal 4:42-44
[d]37 Dinari moja ilikuwa kama mshahara wa kibarua wa siku moja; hivyo dinari 200 ni sawa na mshahara wa siku 200.
[e]**6:38** Mt 15:34; Mk 8:5
[f]**6:41** Mt 14:19
[g]**6:43** Kum 28:5

*Yesu Atembea Juu Ya Maji*

**(Mathayo 14:22-33; Yohana 6:15-21)**

45 [h]Mara Yesu akawaambia wanafunzi wake waingie kwenye mashua watangulie kwenda Bethsaida, wakati yeye alikuwa akiwaaga wale makutano. 46 [i]Baada ya kuwaaga wale watu, akaenda mlimani kuomba.

47 [j]Ilipofika jioni, ile mashua ilikuwa imefika katikati ya bahari, na Yesu alikuwa peke yake katika nchi kavu. 48 [k]Akawaona wanafunzi wake wanahangaika na kupiga makasia kwa nguvu, kwa sababu upepo ulikuwa wa mbisho. Wakati wa zamu ya nne ya usiku, Yesu akawaendea wanafunzi wake, akiwa anatembea juu ya maji. Alikuwa karibu kuwapita, 49 [l]lakini walipomwona akitembea juu ya maji, wakadhani ni mzimu. Wakapiga yowe, 50 [m]kwa sababu wote walipomwona waliogopa.

Mara Yesu akasema nao, akawaambia, “Jipeni moyo! Ni mimi. Msiogope!” 51 [n]Akapanda ndani ya mashua nao, na ule upepo ukakoma! Wakashangaa kabisa, 52 [o]kwa kuwa walikuwa hawajaelewa kuhusu ile mikate. Mioyo yao ilikuwa migumu.

53 [p]Walipokwisha kuvuka, wakafika nchi ya Genesareti, wakatia nanga. 54 Mara waliposhuka kutoka mashua yao, watu wakamtambua Yesu. 55 Wakaenda katika vijiji vyote upesi, wakawabeba wagonjwa kwenye mikeka ili kuwapeleka mahali popote waliposikia kuwa Yesu yupo. 56 [q]Kila mahali Yesu alipokwenda, iwe vijijini, mijini au mashambani, watu waliwaweka wagonjwa wao masokoni. Wakamwomba awaruhusu hao wagonjwa waguse japo upindo wa vazi lake. Nao wote waliomgusa waliponywa.

[h]**6:45** Mt 11:21
[i]**6:46** Lk 3:21
[j]**6:47** Mt 14:23; Yn 6:16, 17
[k]**6:48** Lk 24:28
[l]**6:49** Lk 24:27
[m]**6:50** Lk 14:27
[n]**6:51** Mk 6:32; 4:39
[o]**6:52** Mk 8:17-21
[p]**6:53** Yn 6:24-25
[q]**6:56** Mt 9:20; Mk 5:27, 28; Mdo 19:12

*Kilicho Safi Na Kilicho Najisi*

**(Mathayo 15:1-20)**

7 [a]Mafarisayo na baadhi ya walimu
wa sheria waliokuwa wametoka
Yerusalemu wakakusanyika mbele ya Yesu.
2 [b]Wakawaona baadhi ya wanafunzi wake
wakila chakula kwa mikono iliyo najisi,
yaani, bila kunawa kama ilivyotakiwa na
sheria ya dini ya Wayahudi. 3 [c](Kwa kuwa
Mafarisayo na Wayahudi wote hawali
chakula pasipo kunawa kwa kufuata
desturi za wazee wao. 4 [d]Wanapotoka sokoni
hawawezi kula pasipo kunawa. Pia kuna
desturi nyingine nyingi wanazofuata kama
vile jinsi ya kuosha vikombe, vyungu na
vyombo vya shaba.)

5 [e]Kwa hiyo wale Mafarisayo na walimu
wa sheria wakamuuliza Yesu, “Mbona
wanafunzi wako hawafuati desturi za
wazee, na badala yake wanakula kwa
mikono najisi?”

6 [f]Yesu akawajibu, “Nabii Isaya alisema
ukweli alipotabiri juu yenu, ninyi wanafiki.
Kama ilivyoandikwa:

“ ‘Watu hawa huniheshimu kwa
midomo yao,
lakini mioyo yao iko mbali nami.
7 [g]Huniabudu bure,
nayo mafundisho yao ni maagizo
ya wanadamu tu.’

8 [h]Ninyi mmeziacha amri za Mungu na
kushika desturi za watu.”

9 [i]Naye akawaambia, “Ninyi mnayo njia
nzuri ya kukataa amri za Mungu ili mpate
kuyashika mapokeo yenu! 10 [j]Kwa mfano,
Mose alisema, ‘Waheshimu baba yako
na mama yako,’ na, ‘Yeyote amtukanaye
baba yake au mama yake, na auawe.’
11 [k]Lakini ninyi mwafundisha kwamba mtu
akimwambia baba yake au mama yake,
‘Kile ambacho ningeweza kukusaidia ni
Korbani’ (yaani kimewekwa wakfu kwa
Mungu), 12 basi hawajibiki tena kumsaidia
baba yake au mama yake. 13 [l]Kwa njia
hiyo ninyi mnabatilisha neno la Mungu
kwa mapokeo yenu mliyojiwekea. Nanyi
mnafanya mambo mengi ya aina hiyo.”

14 [m]Yesu akaita tena ule umati wa watu,
akawaambia, “Nisikilizeni, kila mmoja
wenu na mwelewe jambo hili. 15 [n]Hakuna
kitu kinachomwingia mtu kimtiacho unajisi,
lakini kile kimtokacho ndicho kimtiacho
unajisi. [ 16 [o]Kama mtu yeyote ana masikio
ya kusikia na asikie.]”

17 [p]Akiisha kuuacha ule umati wa
watu na kuingia ndani, wanafunzi wake
wakamuuliza maana ya mfano ule.
18 Akawajibu, “Je, hata nanyi hamwelewi?
Je, hamfahamu kwamba kitu kimwingiacho
mtu hakimtii unajisi? 19 [q]Mtu akila kitu
hakiingii moyoni mwake bali tumboni,
na baadaye hutolewa nje ya mwili wake.”
(Kwa kusema hivi, Yesu alivihalalisha
vyakula vyote kuwa ni “safi.”)

20 Akaendelea kusema, “Kile kimtokacho
mtu ndicho kimtiacho unajisi. 21 [r]Kwa
maana kutoka ndani ya moyo wa mtu
hutoka mawazo mabaya, uasherati, wizi,
uuaji, uzinzi, 22 [s]tamaa mbaya, uovu,
udanganyifu, ufisadi, wivu, matukano,
kiburi na upumbavu. 23 Maovu haya yote
hutoka ndani ya mtu, nayo ndiyo yamtiayo
mtu unajisi.”

*Imani Ya Mwanamke Msirofoinike*

**(Mathayo 15:21-28)**

24 [t]Ndipo Yesu akaondoka hapo akaenda
sehemu za Tiro. Akaingia katika nyumba

---

[a]**7:1** Mt 15:1
[b]**7:2** Mdo 11:8; Rum 14:14
[c]**7:3** Mk 7:5-13; Lk 11:38-39
[d]**7:4** Mt 23:25
[e]**7:5** Gal 1:14; Kol 2:8
[f]**7:6** Isa 29:13; Mt 15:8
[g]**7:7** Isa 29:13
[h]**7:8** Mk 7:3
[i]**7:9** Mk 7:3
[j]**7:10** Kut 20:21; Kum 5:16; Kut 21:17; Law 20:9
[k]**7:11** Mt 23:16-18
[l]**7:13** Ebr 4:12; Mk 7:3
[m]**7:14** Mt 15:10
[n]**7:15** Mdo 10:14, 15
[o]**7:16** Mt 11:15
[p]**7:17** Mk 9:28
[q]**7:19** Kol 2:16; 1Tim 4:3-5; Mdo 10:15
[r]**7:21** Mwa 6:5; 8:21; Mt 15:21-28
[s]**7:22** Mt 20:15
[t]**7:24** Mt 21:21

moja, naye hakutaka mtu yeyote ajue kwamba yuko humo. Lakini hakuweza kujificha. 25 [a]Mara mwanamke mmoja, ambaye binti yake mdogo alikuwa na pepo mchafu, akaja na kumpigia magoti miguuni pake. 26 Basi huyo mwanamke alikuwa Myunani, aliyezaliwa Foinike ya Siria.[b] Akamsihi Yesu amtoe binti yake huyo pepo mchafu.

27 Yesu akamwambia, "Waache watoto washibe kwanza, kwa maana si vyema kuchukua chakula cha watoto na kuwatupia mbwa."

28 Lakini yule mwanamke akamjibu, "Bwana, hata mbwa walio chini ya meza hula makombo ya chakula cha watoto."

29 Ndipo Yesu akamjibu, "Kwa sababu ya jibu lako, nenda zako nyumbani; yule pepo mchafu amemtoka binti yako."

30 Akaenda zake nyumbani akamkuta binti yake amelala kitandani, yule pepo mchafu akiwa amemtoka.

### *Yesu Amponya Mtu Aliyekuwa Kiziwi Na Bubu*

31 [c]Kisha Yesu akaondoka sehemu za Tiro, akapita katikati ya Sidoni, hadi Bahari ya Galilaya na kuingia eneo la Dekapoli. 32 [d]Huko, watu wakamletea Yesu mtu mmoja kiziwi, ambaye pia alikuwa na kigugumizi, wakamwomba aweke mkono wake juu ya huyo mtu na amponye.

33 [e]Baadaye Yesu akampeleka yule kiziwi kando mbali na watu, Yesu akatia vidole vyake masikioni mwa yule mtu. Kisha akatema mate na kuugusa ulimi wa yule mtu. 34 [f]Ndipo Yesu akatazama mbinguni, akavuta hewa ndani kwa nguvu akamwambia, *"Efatha!"* (yaani, "Funguka!") 35 [g]Mara masikio yake yakafunguka na ulimi wake ukaachiliwa, akaanza kuongea sawasawa.

36 [h]Yesu akawaamuru wasimwambie mtu yeyote habari hizi. Lakini kadiri alivyowazuia, ndivyo walivyozidi kutangaza kwa bidii. 37 [i]Walistaajabu mno. Wakasema, "Amefanya mambo yote vizuri mno! Amewawezesha viziwi wasikie na bubu waseme!"

### *Yesu Alisha Wanaume 4,000*

**(Mathayo 15:32-39)**

8 [j]Katika siku hizo, umati mkubwa wa watu ulikusanyika tena. Kwa kuwa walikuwa hawana chakula, Yesu akawaita wanafunzi wake akawaambia, 2 [k]"Ninauhurumia huu umati wa watu, kwa sababu sasa wamekuwa nami kwa muda wa siku tatu na hawana chakula. 3 Nikiwaaga waende nyumbani bila kula, watazimia njiani kwa sababu baadhi yao wametoka mbali."

4 Wanafunzi wake wakamjibu, "Lakini hapa nyikani tutapata wapi mikate ya kutosha kuwalisha?"

5 [l]Yesu akawauliza, "Mna mikate mingapi?"

Wakajibu, "Tuna mikate saba."

6 Akawaambia watu waketi chini. Akiisha kuichukua mikate saba na kushukuru, akaimega na kuwapa wanafunzi wake ili wawagawie watu. Wanafunzi wake wakafanya hivyo. 7 [m]Walikuwa pia na visamaki vichache, Yesu akavibariki, akawaamuru wanafunzi wake wawagawie watu. 8 [n]Wale watu walikula na kutosheka. Baadaye wanafunzi wakakusanya vipande vilivyosalia, wakajaza vikapu saba. 9 Watu waliokula walikuwa wapata 4,000. Akiisha kuwaaga, 10 [o]aliingia kwenye mashua pamoja na wanafunzi wake, akaenda sehemu za Dalmanutha.

---

[a]**7:25** Mt 4:24
[b]26 Kulikuwa na Foinike ya Siria (ndio Shamu) na Foinike ya Libya.
[c]**7:31** Mt 11:21; 4:18-25; Mk 5:20
[d]**7:32** Mt 9:32; Lk 11:14; Mk 5:23
[e]**7:33** Mk 8:23
[f]**7:34** Mk 6:41; Yn 11:41; Mk 8:12
[g]**7:35** Isa 35:5-6
[h]**7:36** Mt 8:4
[i]**7:37** Isa 35:5
[j]**8:1** Mt 15:32
[k]**8:2** Mt 9:36
[l]**8:5** Mt 15:34; Mk 6:38
[m]**8:7** Mt 14:19
[n]**8:8** Mk 8:20
[o]**8:10** Mt 15:39

*Mafarisayo Waomba Ishara*

**(Mathayo 12:38-42; 16:1-4)**

11 [a]Mafarisayo wakaja, wakaanza
kumhoji Yesu. Ili kumtega, wakamwomba
awaonyeshe ishara kutoka mbinguni.
12 [b]Akahuzunika moyoni, akawaambia,
"Kwa nini kizazi hiki kinataka ishara? Amin
nawaambieni, hakitapewa ishara yoyote."
13 Kisha akawaacha, akarudi kwenye
mashua, akavuka hadi ng'ambo.

*Chachu Ya Mafarisayo Na Ya Herode*

**(Mathayo 16:5-12)**

14 [c]Wanafunzi walikuwa wamesahau
kuchukua mikate ya kutosha. Walikuwa na
mkate mmoja tu kwenye mashua. 15 [d]Yesu
akawaonya: "Jihadharini na chachu ya
Mafarisayo na ya Herode."

16 [e]Wakajadiliana wao kwa wao, na
kusema, "Anasema hivi kwa sababu
hatukuleta mikate."

17 [f]Yesu, akifahamu majadiliano yao,
akawauliza: "Mbona mnajadiliana kuhusu
kutokuwa na mikate? Je, bado hamtambui
wala hamwelewi? Je, mbona mioyo
yenu ni migumu kiasi hicho? 18 [g]Je, mna
macho lakini mnashindwa kuona, na mna
masikio lakini mnashindwa kusikia? Je,
hamkumbuki? 19 [h]Nilipoimega ile mikate
mitano kuwalisha watu 5,000, mlikusanya
vikapu vingapi vilivyojaa vya masazo?"

Wakamjibu, "Kumi na viwili."

20 [i]"Je, nilipoimega ile mikate saba
kuwalisha watu 4,000, mlikusanya vikapu
vingapi vilivyojaa vya masazo?"

Wakamjibu, "Saba."

21 [j]Ndipo akawauliza, "Je, bado
hamwelewi?"

*Yesu Amponya Kipofu Huko Bethsaida*

22 [k]Wakafika Bethsaida na baadhi ya watu
wakamleta mtu mmoja kipofu wakamsihi
Yesu amguse. 23 [l]Yesu akamshika mkono
huyo kipofu akampeleka nje ya kijiji. Baada
ya kuyatemea mate macho ya yule kipofu
na kumwekea mikono, Yesu akamuuliza,
"Unaona chochote?"

24 Yule kipofu akaangalia, akasema,
"Ninaona watu, wanaonekana kama miti
inayotembea."

25 Yesu akamwekea tena mikono
machoni. Kisha macho yake yakafunguka,
kuona kwake kukarejea naye akaona kila
kitu dhahiri. 26 [m]Yesu akamuaga aende
nyumbani kwake, akimwambia, "Hata
kijijini usiingie."

*Petro Amkiri Yesu Kuwa Ndiye Kristo*

**(Mathayo 16:13-20; Luka 9:18-21)**

27 [n]Yesu na wanafunzi wake wakaondoka
kwenda katika vijiji vya Kaisaria-Filipi.
Walipokuwa njiani, Yesu akawauliza,
"Watu husema mimi ni nani?"

28 [o]Wakamjibu, "Baadhi husema wewe
ni Yohana Mbatizaji, wengine husema ni
Eliya, na bado wengine husema wewe ni
mmojawapo wa manabii."

29 [p]Akawauliza, "Je, ninyi mnasema mimi
ni nani?"

Petro akajibu, "Wewe ndiwe Kristo."[q]

30 [r]Yesu akawaonya wasimwambie mtu
yeyote habari zake.

*Yesu Atabiri Kifo Chake*

**(Mathayo 16:21-28; Luka 9:22-27)**

31 [s]Ndipo akaanza kuwafundisha
wanafunzi wake kuwa Mwana wa Adamu
lazima atapata mateso mengi na kukataliwa
na wazee, viongozi wa makuhani, na

---

[a]**8:11** Mt 12:38
[b]**8:12** Mk 7:34
[c]**8:14** Mt 16:5
[d]**8:15** 1Kor 5:6-8; Lk 12:1; Mt 14:1; Mk 12:13
[e]**8:16** Mt 16:7
[f]**8:17** Isa 6:9-10; Mk 6:52
[g]**8:18** Yer 5:21; Eze 12:2
[h]**8:19** Lk 9:17; Yn 6:13
[i]**8:20** Mk 8:6-9; Mt 15:37
[j]**8:21** Mk 6:52
[k]**8:22** Mt 11:21; Mk 10:46; Yn 9:1
[l]**8:23** Mk 7:33; 5:23
[m]**8:26** Mt 8:14; Mk 5:43
[n]**8:27** Mt 16:13; Lk 9:18
[o]**8:28** Mt 3:1; Mal 4:5
[p]**8:29** Yn 6:69; 11:27
[q]29 *Kristo* maana yake ni *Masiya*, yaani *Aliyetiwa mafuta.*
[r]**8:30** Mt 17:9; Lk 9:21
[s]**8:31** Mt 8:20; 16:21; 27:1-2; Mdo 2:23

walimu wa sheria, na kwamba itampasa
auawe lakini baada ya siku tatu afufuke.
32 [a]Aliyasema haya waziwazi, ndipo Petro
akamchukua kando na akaanza kumkemea.
33 [b]Lakini Yesu alipogeuka na kuwaangalia
wanafunzi wake, akamkemea Petro.
Akasema, “Rudi nyuma yangu, Shetani!
Moyo wako hauwazi yaliyo ya Mungu, bali
ya wanadamu.”
34 [c]Ndipo akauita ule umati wa watu
pamoja na wanafunzi wake, akasema, “Mtu
yeyote akitaka kunifuata, ni lazima ajikane
mwenyewe, auchukue msalaba wake,
anifuate. 35 [d]Kwa maana yeyote anayetaka
kuyaokoa maisha yake atayapoteza, lakini
yeyote atakayeyapoteza maisha yake kwa
ajili yangu na kwa ajili ya Injili atayaokoa.
36 Je, itamfaidi nini mtu kuupata ulimwengu
wote, lakini akayapoteza maisha yake?
37 Au mtu atatoa nini badala ya nafsi
yake? 38 [e]Mtu yeyote akinionea aibu mimi
na maneno yangu katika kizazi hiki cha
uzinzi na dhambi, Mwana wa Adamu naye
atamwonea aibu wakati atakapokuja katika
utukufu wa Baba yake pamoja na malaika
watakatifu.”

9 [f]Yesu akaendelea kuwaambia, “Amin,
nawaambia, kuna watu waliosimama
hapa ambao hawataonja mauti kabla
ya kuuona Ufalme wa Mungu ukija kwa
nguvu.”

*Yesu Ageuka Sura*

**(Mathayo 17:1-13; Luka 9:28-36)**

2 [g]Baada ya siku sita, Yesu akawachukua
Petro, Yakobo na Yohana, akawapeleka
juu ya mlima mrefu, mahali walipokuwa
faraghani. Huko, Yesu akageuka sura mbele
yao. 3 [h]Mavazi yake yakawa na weupe wa
kuzima macho, meupe kuliko ambavyo mtu
yeyote duniani angaliweza kuyang’arisha.
4 Mose na Eliya wakawatokea, wakawa
wanazungumza na Yesu.
5 [i]Petro akamwambia Yesu, “Rabi, ni
vyema sisi tukae hapa. Turuhusu tujenge
vibanda vitatu: kimoja chako, kingine cha
Mose na kingine cha Eliya.” 6 Petro hakujua
aseme nini kwa maana yeye na wenzake
walikuwa wameogopa sana.
7 [j]Ndipo pakatokea wingu, likawafunika,
nayo sauti kutoka lile wingu ikasema,
“Huyu ni Mwanangu mpendwa. Msikieni
yeye.”
8 Mara walipotazama huku na huku,
hawakuona tena mtu mwingine yeyote
pamoja nao isipokuwa Yesu.
9 [k]Walipokuwa wakishuka kutoka
mlimani, Yesu akawakataza wasimwambie
mtu yeyote mambo waliyoona, mpaka
Mwana wa Adamu atakapokuwa amefufuka
kutoka kwa wafu. 10 Wakalihifadhi jambo
hilo wao wenyewe, lakini wakawa
wanajiuliza, “Huku kufufuka kwa wafu
maana yake nini?”
11 [l]Wakamuuliza, “Kwa nini walimu wa
sheria husema kwamba ni lazima Eliya aje
kwanza?”
12 [m]Yesu akawajibu, “Ni kweli, Eliya
yuaja kwanza ili kutengeneza mambo
yote. Mbona basi imeandikwa kwamba
Mwana wa Adamu ni lazima ateseke sana
na kudharauliwa? 13 [n]Lakini ninawaambia,
Eliya amekwisha kuja, nao wakamtendea
walivyopenda, kama ilivyoandikwa
kumhusu yeye.”

*Mvulana Mwenye Pepo Mchafu Aponywa*

**(Mathayo 17:14-21; Luka 9:37-43)**

14 [o]Walipowafikia wale wanafunzi
wengine, wakawakuta wamezungukwa
na umati mkubwa wa watu na baadhi
ya walimu wa sheria wakibishana nao.
15 Mara wale watu walipomwona Yesu,

[a]**8:32** Yn 18:20
[b]**8:33** Mt 4:10
[c]**8:34** Mt 10:38; Lk 14:27
[d]**8:35** Yn 12:25
[e]**8:38** Mt 8:20; 10:33; Lk 12:9; 1The 2:19
[f]**9:1** Mk 13:30; Lk 22:18; Mt 24:30; 25:30
[g]**9:2** Mt 4:21
[h]**9:3** Mt 28:3
[i]**9:5** Mt 23:7
[j]**9:7** Kut 24:16; Mt 3:17
[k]**9:9** Mk 8:20-30
[l]**9:11** Mal 4:5; Mt 17:10
[m]**9:12** Mt 8:20; 16:21; Lk 13:11
[n]**9:13** Mt 11:14
[o]**9:14** Mt 17:14; Lk 9:37; 9:1-20; Mt 17:14-21

wakastaajabu sana, wakamkimbilia ili kumsalimu.
16 Akawauliza wanafunzi wake, “Mnabishana nao kuhusu nini?”
17 [a]Mtu mmoja miongoni mwa ule umati wa watu akajibu, “Mwalimu, nilimleta kwako mwanangu ambaye ana pepo mchafu anayemfanya asiweze kuongea. 18 Kila mara huyo pepo mchafu ampagaapo mwanangu, humwangusha chini na kumfanya atokwe povu mdomoni na kusaga meno, kisha mwili wake hukauka. Niliwaomba wanafunzi wako wamtoe huyo pepo mchafu, lakini hawakuweza.”
19 Yesu akawaambia, “Enyi kizazi kisicho na imani! Nitakuwa pamoja nanyi mpaka lini? Nitawavumilia mpaka lini? Mleteni mvulana kwangu.”
20 [b]Nao wakamleta yule mvulana. Yule pepo mchafu alipomwona Yesu, mara akamtia yule mvulana kifafa, akaanguka, akagaagaa chini huku akitokwa na povu kinywani.
21 Yesu akamuuliza baba yake, “Mwanao amekuwa katika hali hii tangu lini?”
Akamjibu, “Tangu utoto wake. 22 Mara kwa mara huyo pepo mchafu amekuwa akimwangusha kwenye moto au kwenye maji ili kumwangamiza. Lakini kama unaweza kufanya jambo lolote, tafadhali tuhurumie utusaidie.”
23 [c]Yesu akamwambia, “Kama ukiweza kuamini, yote yawezekana kwake yeye aaminiye.”
24 [d]Mara baba yake yule mvulana akapiga kelele akisema, “Ninaamini. Nisaidie kutokuamini kwangu!” 25 [e]Yesu alipoona kwamba umati wa watu unakusanyika pamoja mbio, akamkemea yule pepo mchafu, akimwambia, “Wewe pepo bubu na kiziwi, nakuamuru umtoke, wala usimwingie tena!”
26 Yule pepo mchafu akiisha kupiga kelele, akamtia kifafa kwa nguvu, na akamtoka. Yule mvulana alikuwa kama maiti, hivyo
watu wengi wakasema, “Amekufa.” 27 Lakini Yesu akamshika mkono, akamwinua, naye akasimama.
28 [f]Baada ya Yesu kuingia ndani ya nyumba, wanafunzi wake wakamuuliza wakiwa peke yao, “Mbona sisi hatukuweza kumtoa huyo pepo mchafu?”
29 Yesu akawajibu, “Hali hii haiwezi kutoka isipokuwa kwa kuomba na kufunga.”

### *Yesu Atabiri Tena Kifo Chake Na Ufufuo*

**(Mathayo 17:22-23; Luka 9:43-45)**

30 [g]Wakaondoka huko, wakapitia Galilaya. Yesu hakutaka mtu yeyote afahamu mahali walipo, 31 [h]kwa maana alikuwa anawafundisha wanafunzi wake. Akawaambia, “Mwana wa Adamu atasalitiwa na kutiwa mikononi mwa watu. Nao watamuua, lakini siku tatu baada ya kuuawa atafufuka.” 32 [i]Lakini wao hawakuelewa kile alimaanisha, nao waliogopa kumuuliza maana yake.

### *Mabishano Kuhusu Aliye Mkuu Zaidi*

**(Mathayo 18:1-5; Luka 9:46-48)**

33 [j]Basi wakafika Kapernaumu na baada ya kuingia nyumbani akawauliza, “Mlikuwa mnabishana nini kule njiani?” 34 [k]Lakini hawakumjibu, kwa sababu njiani walikuwa wakibishana kuhusu nani miongoni mwao alikuwa mkuu zaidi ya wote.
35 [l]Akaketi chini, akawaita wote kumi na wawili, akawaambia: “Kama mtu yeyote akitaka kuwa wa kwanza, hana budi kuwa wa mwisho na mtumishi wa wote.”
36 [m]Kisha akamchukua mtoto mdogo, akamsimamisha katikati yao. Akamkumbatia, akawaambia, 37 [n]“Mtu yeyote amkaribishaye mmoja wa hawa watoto wadogo kwa Jina langu, anikaribisha

[a]**9:17** Mt 17:14; Lk 9:38
[b]**9:20** Mk 1:26
[c]**9:23** Mt 21:21; Yn 11:40
[d]**9:24** Lk 17:5
[e]**9:25** Mk 9:15; 1:26
[f]**9:28** Mk 7:17; Mt 17:19
[g]**9:30** Yn 7:1
[h]**9:31** Mt 8:20; Mdo 2:23; 3:13; Mt 16:21
[i]**9:32** Lk 18:34; Yn 12:16
[j]**9:33** Mt 4:13; Mk 1:29
[k]**9:34** Lk 22:24
[l]**9:35** Mt 20:26; Lk 22:26
[m]**9:36** Mk 10:16
[n]**9:37** Mt 10:40

mimi. Naye anikaribishaye mimi,
amkaribisha Baba yangu aliyenituma."

### *Yeyote Asiye Kinyume Nasi Yuko Upande Wetu*

**(Luka 9:49-50)**

38 [a]Yohana akamwambia, "Mwalimu,
tumemwona mtu akitoa pepo wachafu kwa
jina lako, nasi tukamkataza, kwa sababu
yeye si mmoja wetu."
39 [b]Yesu akasema, "Msimkataze, kwa
kuwa hakuna yeyote atendaye miujiza kwa
Jina langu ambaye baada ya kitambo kidogo
aweza kunena lolote baya dhidi yangu.
40 [c]Kwa maana yeyote asiye kinyume chetu,
yuko upande wetu. 41 [d]Amin, nawaambia,
yeyote awapaye ninyi kikombe cha maji
kwa Jina langu kwa sababu ninyi ni mali
ya Kristo, hakika hataikosa thawabu yake."

### *Kusababisha Kutenda Dhambi*

**(Mathayo 18:6-9; Luka 17:1-2)**

42 [e]"Kama mtu yeyote akimsababisha
mmojawapo wa wadogo hawa wanaoniamini
kutenda dhambi, ingekuwa bora kwake
afungiwe jiwe kubwa la kusagia shingoni
mwake, na kutoswa baharini. 43 [f]Kama
mkono wako ukikusababisha kutenda
dhambi, ukate. Ni afadhali kwako kuingia
katika uzima ukiwa na mkono mmoja, kuliko
kuwa na mikono miwili lakini ukaingia
jehanamu, mahali ambako moto hauzimiki.
[ 44 [g]Mahali ambako funza wake hawafi wala
moto wake hauzimiki.] 45 [h]Kama mguu wako
ukikusababisha kutenda dhambi, ukate. Ni
afadhali kwako kuingia katika uzima ukiwa
kiwete, kuliko kuwa na miguu miwili lakini
ukaingia jehanamu. [ 46 Mahali ambako
funza wake hawafi wala moto hauzimiki.]
47 [i]Nalo jicho lako likikusababisha kutenda
dhambi, ling'oe. Ni afadhali kwako kuingia
katika Ufalme wa Mungu ukiwa na jicho
moja, kuliko kuwa na macho mawili lakini
ukatupwa jehanamu, 48 [j]mahali ambako

" 'funza wake hawafi,
wala moto wake hauzimiki.'

49 [k]Kila mmoja atatiwa chumvi kwa moto.
50 [l]"Chumvi ni nzuri, lakini ikipoteza
ladha yake utaifanyaje ili iweze kukolea
tena? Mwe na chumvi ndani yenu, mkaishi
kwa amani, kila mmoja na mwenzake."

### *Mafundisho Kuhusu Talaka*

**(Mathayo 19:1-12; Luka 16:18)**

10 [m]Yesu akaondoka huko, akavuka Mto
Yordani, akaenda sehemu za Uyahudi.
Umati mkubwa wa watu ukaenda kwake
tena, naye kama ilivyokuwa desturi yake,
akawafundisha.
2 [n]Baadhi ya Mafarisayo wakaja ili
kumjaribu kwa kumuuliza, "Je, ni halali
mtu kumwacha mke wake?"
3 Yesu akawajibu, "Je, Mose aliwaamuru
nini?"
4 [o]Wakajibu, "Mose aliruhusu kwamba
mume anaweza kumwandikia mkewe hati
ya talaka na kumwacha."
5 [p]Yesu akawaambia, "Mose aliwaandikia
sheria hiyo kwa sababu ya ugumu wa
mioyo yenu. 6 [q]Lakini tangu mwanzo wa
uumbaji, 'Mungu aliwaumba mwanaume na
mwanamke. 7 [r]Kwa sababu hii mwanaume
atamwacha baba yake na mama yake na
kuambatana na mkewe, na hao wawili
watakuwa mwili mmoja.' 8 [s]Kwa hiyo
hawatakuwa wawili tena, bali mwili
mmoja. 9 Basi, alichokiunganisha Mungu,
mwanadamu asikitenganishe."
10 Walipokuwa tena ndani ya nyumba,
wanafunzi wake wakamuuliza kuhusu

[a]**9:38** Hes 11:27-29
[b]**9:39** 1Kor 12:3
[c]**9:40** Mt 12:30; Lk 11:23
[d]**9:41** Mt 10:42
[e]**9:42** Mt 5:29; 18:6; Lk 17:2
[f]**9:43** Mt 5:29-30; 18:8; 25:41
[g]**9:44** Isa 66:24
[h]**9:45** Mt 5:29; 18:8
[i]**9:47** Mt 5:29; 18:9
[j]**9:48** Isa 66:24; Mt 25:41
[k]**9:49** Law 2:13
[l]**9:50** Mt 5:13; Lk 14:34-35; Kol 4:6; Rum 12:18; 1The 5:13
[m]**10:1** Yn 10:40; 11:7; Mt 4:23; Mk 4:2
[n]**10:2** Mk 2:16
[o]**10:4** Kum 24:1-4; Mt 5:31
[p]**10:5** Za 95:8; Ebr 3:15
[q]**10:6** Mwa 1:27; 5:2
[r]**10:7** Mwa 2:2; 1Kor 6:16; Efe 5:31
[s]**10:8** Mwa 2:24; 1Kor 6:16

jambo hili. 11 [a]Akawajibu, “Mtu yeyote
amwachaye mkewe na kuoa mke mwingine,
anazini naye. 12 [b]Naye mwanamke
amwachaye mumewe na kuolewa na mume
mwingine, anazini.”

*Yesu Anawabariki Watoto Wadogo*

### (Mathayo 19:13-15; Luka 18:15-17)

13 [c]Watu walikuwa wakimletea Yesu
watoto wadogo ili awaguse, lakini
wanafunzi wake wakawakemea.
14 [d]Yesu alipoona yaliyokuwa yakitukia,
akachukizwa. Akawaambia wanafunzi
wake, “Waacheni watoto wadogo waje
kwangu, wala msiwazuie, kwa maana
Ufalme wa Mungu ni wa wale walio
kama hawa. 15 [e]Amin, nawaambia, mtu
yeyote asiyeupokea Ufalme wa Mungu
kama mtoto mdogo, hatauingia kamwe.”
16 [f]Akawachukua watoto mikononi mwake,
akawakumbatia, akaweka mikono yake juu
yao, akawabariki.

*Kijana Tajiri*

### (Mathayo 19:16-30; Luka 18:18-30)

17 [g]Yesu alipokuwa anaondoka, mtu
mmoja akamkimbilia, akapiga magoti
mbele yake, akamuuliza, “Mwalimu
mwema, nifanye nini ili niurithi uzima wa
milele?”
18 Yesu akamwambia, “Mbona unaniita
mwema? Hakuna yeyote aliye mwema
ila Mungu peke yake. 19 [h]Unazijua amri:
‘Usiue, usizini, usiibe, usishuhudie uongo,
usidanganye, waheshimu baba yako na
mama yako.’ ”
20 Akamjibu, “Mwalimu, amri hizi zote
nimezishika tangu nikiwa mtoto.”
21 [i]Yesu akamtazama na kumpenda,
akamwambia, “Umepungukiwa na kitu
kimoja. Nenda ukauze kila kitu ulicho
nacho uwape maskini hizo fedha, nawe
utakuwa na hazina mbinguni. Kisha njoo,
unifuate.”
22 Yule mtu aliposikia hayo, akasikitika
sana. Akaondoka kwa huzuni kwa sababu
alikuwa na mali nyingi.
23 [j]Yesu akatazama pande zote,
akawaambia wanafunzi wake, “Itakuwa
vigumu sana kwa wenye mali kuingia
katika Ufalme wa Mungu!”
24 [k]Wanafunzi wake wakashangazwa sana
na maneno hayo. Lakini Yesu akawaambia
tena, “Wanangu, tazama jinsi ilivyo vigumu
kwa wale wanaotumainia mali kuingia
katika Ufalme wa Mungu. 25 [l]Ni rahisi
zaidi kwa ngamia kupita kwenye tundu la
sindano kuliko mtu tajiri[m] kuingia katika
Ufalme wa Mungu.”
26 Wanafunzi wake wakashangaa sana.
Wakaulizana wao kwa wao, “Ni nani basi
awezaye kuokoka?”
27 [n]Yesu akawatazama, akawaambia,
“Kwa mwanadamu jambo hili haliwezekani,
lakini kwa Mungu sivyo. Mambo yote
yanawezekana kwa Mungu.”
28 [o]Ndipo Petro akamjibu, “Tazama,
tumeacha kila kitu na kukufuata wewe!”
29 Yesu akasema, “Amin, nawaambia,
hakuna mtu yeyote aliyeacha nyumba,
ndugu wa kiume au wa kike, au mama au
baba, au watoto au mashamba kwa ajili
yangu na kwa ajili ya Injili, 30 [p]ambaye
hatalipwa mara mia katika ulimwengu
huu: nyumba, ndugu wa kiume na wa
kike, mama na baba na watoto, mashamba
pamoja na mateso, kisha uzima wa milele
katika ulimwengu ujao. 31 [q]Lakini wengi
walio wa kwanza watakuwa wa mwisho,
na wa mwisho watakuwa wa kwanza.”

---

[a] **10:11** Mt 5:32; Lk 16:8
[b] **10:12** Rum 7:3; 1Kor 7:10-11
[c] **10:13** Mt 19:13; Lk 18:15
[d] **10:14** Mt 25:34
[e] **10:15** Mt 18:3
[f] **10:16** Mk 9:36
[g] **10:17** Mk 1:40; Lk 10:25; Mdo 20:32
[h] **10:19** Kut 20:12-16; Kum 5:16-20
[i] **10:21** Mdo 2:45; Mt 6:20; Lk 12:33; Mt 4:19
[j] **10:23** Za 62:10; 1Tim 6:9-17
[k] **10:24** Mt 7:13-14; Yn 3:5
[l] **10:25** Lk 12:16-20; 16:19-31
[m] 25 Tajiri ina maana wale wanaotumainia mali.
[n] **10:27** Mt 19:26
[o] **10:28** Mt 4:18-19; Lk 18:28
[p] **10:30** Mt 6:33; 12:32; 25:46
[q] **10:31** Mt 19:30

*Yesu Atabiri Mara Ya Tatu Kufa Na Kufufuka Kwake*

**(Mathayo 20:17-19; Luka 18:31-34)**

32 [a]Walikuwa njiani wakipanda kwenda
Yerusalemu, na Yesu alikuwa ametangulia.
Wanafunzi wake walishangaa, nao watu
waliowafuata walijawa na hofu. Yesu
akawachukua tena wale wanafunzi wake
kumi na wawili kando na kuwaambia
yatakayompata. 33 [b]Akasema, "Tunapanda
kwenda Yerusalemu, na Mwana wa Adamu
atasalitiwa kwa viongozi wa makuhani na
walimu wa sheria. Wao watamhukumu kifo
na kumtia mikononi mwa watu wa Mataifa,
34 [c]ambao watamdhihaki na kumtemea
mate, watampiga na kumuua. Siku tatu
baadaye atafufuka."

*Ombi La Yakobo Na Yohana*

**(Mathayo 20:20-28)**

35 [d]Kisha Yakobo na Yohana, wana wa
Zebedayo, wakaja kwake na kumwambia,
"Mwalimu, tunataka utufanyie lolote
tutakalokuomba."
36 Naye akawaambia, "Je, mwataka
niwafanyie jambo gani?"
37 [e]Wakamwambia, "Tupe kukaa mmoja
upande wako wa kuume na mwingine
upande wako wa kushoto katika utukufu
wako."
38 [f]Lakini Yesu akawaambia, "Ninyi
hamjui mnaloliomba. Je, mnaweza
kukinywea kikombe ninyweacho mimi,
au kubatizwa ubatizo nibatizwao mimi?"
39 [g]Wakajibu, "Tunaweza."
Kisha Yesu akawaambia, "Kikombe
nikinyweacho mtakinywea na ubatizo
nibatizwao mtabatizwa, 40 lakini kuketi
mkono wangu wa kuume au wa kushoto
si juu yangu mimi kuwapa. Nafasi hizi ni
kwa ajili ya wale walioandaliwa."
41 [h]Wale wanafunzi wengine kumi
waliposikia hayo, wakaanza kuwakasirikia
Yakobo na Yohana. 42 [i]Lakini Yesu akawaita
wote pamoja na kuwaambia, "Mnafahamu
kuwa wale wanaodhaniwa kuwa watawala
wa watu wa Mataifa huwatawala watu
kwa nguvu, nao wenye vyeo huonyesha
mamlaka yao. 43 [j]Lakini isiwe hivyo kwenu.
Badala yake, yeyote anayetaka kuwa mkuu
miongoni mwenu hana budi kuwa mtumishi
wenu, 44 na yeyote anayetaka kuwa wa
kwanza, hana budi kuwa mtumwa wa
wote. 45 [k]Kwa kuwa hata Mwana wa Adamu
hakuja ili kutumikiwa, bali kutumika na
kuutoa uhai wake uwe fidia kwa ajili ya
wengi."

*Yesu Amponya Kipofu Bartimayo*

**(Mathayo 20:29-34; Luka 18:35-43)**

46 [l]Kisha wakafika Yeriko. Yesu alipokuwa
akiondoka mjini na wanafunzi wake pamoja
na umati mkubwa wa watu, kipofu mmoja,
jina lake Bartimayo, mwana wa Timayo,
alikuwa ameketi kando ya njia akiomba
msaada. 47 [m]Aliposikia kuwa ni Yesu wa
Nazareti aliyekuwa anapita, akaanza
kupaza sauti akisema, "Yesu, Mwana wa
Daudi, nihurumie!"
48 Watu wengi wakamkemea,
wakamwambia akae kimya, lakini yeye
akazidi kupaza sauti, akisema, "Mwana
wa Daudi, nihurumie!"
49 Yesu akasimama na kusema, "Mwiteni."
Hivyo wakamwita yule mtu kipofu,
wakamwambia, "Jipe moyo! Inuka,
anakuita." 50 Akiwa analivua lile joho lake,
alisimama na kumwendea Yesu.
51 [n]Yesu akamuuliza, "Unataka nikufanyie
nini?"
Yule kipofu akajibu, "Mwalimu, nataka
kuona."

[a]**10:32** Mk 3:16-19
[b]**10:33** Lk 9:51; Mt 8:20; 27:1-2
[c]**10:34** Mdo 2:23; Mt 16:21
[d]**10:35** Mt 20:20; 20:20-28
[e]**10:37** Mt 19:28
[f]**10:38** Ay 38:2; Mt 20:22; Lk 12:50
[g]**10:39** Mdo 12:22; Ufu 1:9
[h]**10:41** Mt 20:24
[i]**10:42** Lk 22:25-27
[j]**10:43** Mk 5:35
[k]**10:45** Mt 20:28
[l]**10:46** Mt 20:29; Lk 18:35-43; Mt 20:29-34; Lk 18:35-43
[m]**10:47** Mk 1:24; Mt 9:27
[n]**10:51** Mt 23:7

52 [a]Yesu akamwambia, "Nenda zako, imani yako imekuponya." Mara akapata kuona, akamfuata Yesu njiani.

*Yesu Aingia Yerusalemu Kwa Shangwe*

### (Mathayo 21:1-11; Luka 19:28-40; Yohana 12:12-19)

11 [b]Walipokaribia Yerusalemu, wakafika Bethfage na Bethania katika Mlima wa Mizeituni. Yesu akawatuma wawili
wa wanafunzi wake, 2 [c]akawaambia,
"Nendeni katika kijiji kilichoko mbele yenu. Na hapo mtakapoingia kijijini, mtamkuta mwana-punda amefungwa hapo, ambaye hajapandwa na mtu bado.
Mfungueni, mkamlete hapa. 3 [d]Kama mtu
yeyote akiwauliza, 'Mbona mnamfungua?' Mwambieni, 'Bwana anamhitaji, na atamrudisha hapa baada ya muda mfupi.' "
4 [e]Wakaenda, wakamkuta mwana-punda amefungwa kando ya barabara, karibu
na mlango wa nyumba. 5 Walipokuwa
wanamfungua, watu waliokuwa wamesimama karibu wakawauliza, "Mna maana gani mnapomfungua huyo mwana-
punda?" 6 Wakawajibu kama vile Yesu
alivyokuwa amewaagiza, nao wale watu
wakawaruhusu. 7 Kisha wakamleta huyo
mwana-punda kwa Yesu na kutandika mavazi yao juu yake, naye akampanda.
8 [f]Watu wengi wakatandaza mavazi yao barabarani, na wengine wakatandaza matawi waliyokuwa wamekata
mashambani. 9 [g]Kisha wale waliokuwa wametangulia mbele na wale waliokuwa wakifuata nyuma wakapaza sauti, wakisema,

"Hosana!"[h]

"Amebarikiwa yeye ajaye kwa Jina
la Bwana!"

10 [i]"Umebarikiwa Ufalme unaokuja wa
baba yetu Daudi!"

"Hosana kwake yeye aliye juu!"

11 [j]Yesu akaingia Yerusalemu na kwenda Hekaluni. Akaangalia kila kitu kilichokuwamo, lakini kwa kuwa ilishakuwa jioni, akaenda zake Bethania pamoja na wale kumi na wawili.

*Yesu Alaani Mtini Usiozaa*

### (Mathayo 21:18-19)

12 [k]Kesho yake walipokuwa wakitoka
Bethania, Yesu alikuwa na njaa. 13 Akauona
mtini kwa mbali, naye akaenda ili aone kama ulikuwa na matunda. Alipoufikia, akakuta una majani tu, kwa kuwa
hayakuwa majira ya tini. 14 [l]Akauambia ule
mti, "Tangu leo mtu yeyote asile kamwe matunda kutoka kwako." Wanafunzi wake walimsikia akisema hayo.

*Yesu Atakasa Hekalu*

### (Mathayo 21:12-17; Luka 19:45-48; Yohana 2:13-22)

15 [m]Walipofika Yerusalemu, Yesu akaingia katika eneo la Hekalu, akaanza kuwafukuza wale waliokuwa wakinunua na kuuza humo ndani. Akazipindua meza za wale waliokuwa wakibadilisha fedha, na pia viti vya wale waliokuwa wakiuza njiwa,
16 wala hakumruhusu mtu yeyote kuchukua
bidhaa kupitia ukumbi wa Hekalu. 17 [n]Naye
alipokuwa akiwafundisha, akasema, "Je, haikuandikwa kuwa:

" 'Nyumba yangu itaitwa
nyumba ya sala kwa mataifa
yote'?

[a]**10:52** Mt 9:22; 4:19; Mk 5:34
[b]**11:1** Mt 21:17; 21:1
[c]**11:2** Hes 19:2; 1Sam 6:7
[d]**11:3** Mk 14:14
[e]**11:4** Mk 14:16
[f]**11:8** Mt 21:8
[g]**11:9** Za 118:25-26; Mt 23:39

[h]9 Kiebrania kusema Okoa, basi likawa neno la shangwe.
[i]**11:10** Lk 2:14
[j]**11:11** Mt 21:12-17
[k]**11:12** Mt 21:18
[l]**11:14** Mk 11:20
[m]**11:15** Mt 21:12; Lk 19:45; Yn 2:14
[n]**11:17** Isa 56:7; Yer 7:11

Lakini ninyi mmeifanya kuwa ‘pango la
wanyang’anyi.’ ”
18 [a]Viongozi wa makuhani na walimu
wa sheria wakapata habari hizi, nao
wakaanza kutafuta njia ya kumuua, kwa
kuwa walikuwa wakimwogopa, kwa sababu
umati wote ulikuwa unashangazwa na
mafundisho yake.
19 [b]Ilipofika jioni, Yesu na wanafunzi
wake wakatoka nje ya mji.

*Mtini Ulionyauka*

**(Mathayo 21:20-22)**

20 [c]Asubuhi yake walipokuwa wakipita,
wakauona ule mtini umenyauka kutoka
juu hadi kwenye mizizi yake. 21 [d]Petro
akakumbuka na kumwambia Yesu, “Rabi,
tazama! Ule mtini ulioulaani umenyauka!”
22 [e]Yesu akawajibu, “Mwaminini
Mungu. 23 [f]Amin, nawaambia, mtu yeyote
atakayeuambia mlima huu, ‘Ng’oka
ukatupwe baharini,’ wala asione shaka
moyoni mwake, bali aamini kwamba
hayo asemayo yametukia, atatimiziwa.
24 [g]Kwa sababu hiyo nawaambia, yoyote
mtakayoyaomba mkisali, aminini ya
kwamba mmeyapokea, nayo yatakuwa
yenu. 25 [h]Nanyi kila msimamapo kusali,
sameheni mkiwa na neno na mtu, ili naye
Baba yenu aliye mbinguni awasamehe
ninyi makosa yenu. [ 26 [i]Lakini kama
ninyi msiposamehe, wala Baba yenu aliye
mbinguni hatawasamehe ninyi makosa
yenu.]”

*Swali Kuhusu Mamlaka Ya Yesu*

**(Mathayo 21:23-27; Luka 20:1-8)**

27 [j]Wakafika tena Yerusalemu, na Yesu
alipokuwa akitembea Hekaluni, viongozi
wa makuhani, walimu wa sheria pamoja na
wazee wa watu wakamjia. 28 Wakamuuliza,
“Unafanya mambo haya kwa mamlaka
gani? Na ni nani aliyekupa mamlaka ya
kufanya hayo?”
29 Yesu akawajibu, “Nitawauliza swali
moja. Nijibuni, nami nitawaambia ni kwa
mamlaka gani ninafanya mambo haya.
30 Niambieni, je, ubatizo wa Yohana ulitoka
mbinguni au kwa wanadamu?”
31 Wakahojiana wao kwa wao, wakisema,
“Kama tukisema, ‘Ulitoka mbinguni,’
atatuuliza, ‘Mbona hamkumwamini?’
32 [k]Lakini tukisema, ‘Ulitoka kwa
wanadamu,’…” (Waliwaogopa watu, kwa
sababu kila mtu aliamini kwamba Yohana
alikuwa nabii wa kweli.)
33 Kwa hiyo wakamjibu Yesu, “Hatujui.”
Naye Yesu akawaambia, “Wala mimi
sitawaambia ni kwa mamlaka gani
ninatenda mambo haya.”

*Mfano Wa Wapangaji Waovu*

**(Mathayo 21:33-46; Luka 20:9-19)**

12 [l]Yesu akaanza kusema nao kwa mifano,
akawaambia: “Mtu mmoja alipanda
shamba la mizabibu. Akajenga ukuta
kulizunguka, akachimba shimo ndani
yake kwa ajili ya shinikizo la kusindika
divai, na akajenga mnara wa ulinzi. Kisha
akalikodisha shamba hilo la mizabibu kwa
wakulima fulani, kisha akasafiri kwenda nchi
nyingine. 2 Wakati wa mavuno ulipofika,
mwenye shamba akamtuma mtumishi
wake kwa hao wapangaji ili kuchukua
sehemu yake ya mavuno ya shamba la
mizabibu kutoka kwa hao wapangaji.
3 Lakini wale wakulima walimkamata
yule mtumishi, wakampiga, wakamfukuza
mikono mitupu. 4 Kisha yule mwenye
shamba akamtuma mtumishi mwingine
kwao; nao wale wakulima wakampiga
kichwani na kumfanyia mambo ya aibu.
5 Kisha akamtuma mtumishi mwingine,
naye huyo wakamuua. Akawatuma wengine
wengi; baadhi yao wakawapiga, na wengine
wakawaua.
6 [m]“Mwenye shamba alikuwa bado

[a]**11:18** Mt 21:46; Lk 20:19; Mt 7:28
[b]**11:19** Lk 21:37
[c]**11:20** Mt 21:19; Mk 11:14
[d]**11:21** Mt 23:7
[e]**11:22** Yn 14:1
[f]**11:23** Mt 21:21
[g]**11:24** Mt 7:7
[h]**11:25** Mt 6:14
[i]**11:26** Mt 18:35; 6:4, 15
[j]**11:27** Mt 21:23; Lk 20:1
[k]**11:32** Mt 11:9
[l]**12:1** Isa 5:17
[m]**12:6** Ebr 1:1-3

na mmoja wa kumtuma, mwanawe
aliyempenda. Hatimaye akamtuma akisema,
'Watamheshimu mwanangu.'
7 "Lakini wale wapangaji wakasemezana
pamoja, 'Huyu ndiye mrithi. Njooni
tumuue, nao urithi utakuwa wetu.' 8 [a]Hivyo
wakamchukua na kumuua, wakamtupa nje
ya lile shamba la mizabibu.
9 "Sasa basi yule mwenye shamba
atafanya nini? Atakuja na kuwaua hao
wapangaji, kisha atawapa wapangaji
wengine hilo shamba la mizabibu. 10 [b]Je,
hamjasoma Andiko hili:

" 'Jiwe walilolikataa waashi
limekuwa jiwe kuu la pembeni;
11 [c]Bwana ndiye alitenda jambo hili,
nalo ni ajabu machoni petu'?"

12 [d]Walipotambua kuwa amesema mfano
huo kwa ajili yao, wakataka kumkamata,
lakini wakaogopa ule umati wa watu.
Wakamwacha, wakaondoka, wakaenda zao.

*Swali Kuhusu Kulipa Kodi*

**(Mathayo 22:15-22; Luka 20:20-26)**

13 [e]Baadaye wakawatuma baadhi ya
Mafarisayo na Maherode ili kwenda
kumtega Yesu katika yale anayosema.
14 Wakamjia, wakamwambia, "Mwalimu,
tunajua kwamba wewe ni mtu mwadilifu.
Wewe huyumbishwi na wanadamu, kwa
kuwa huna upendeleo. Lakini wewe
huifundisha njia ya Mungu katika kweli.
Je, ni halali kulipa kodi kwa Kaisari, au
la? 15 Je, tulipe kodi au tusilipe?"
Lakini Yesu alijua unafiki wao. Akawauliza
"Mbona mnajaribu kunitega? Nileteeni hiyo
dinari[f] niione." 16 Wakamletea hiyo sarafu.
Naye akawauliza, "Sura hii ni ya nani? Na
maandishi haya ni ya nani?"
Wakamjibu, "Ni vya Kaisari."
17 [g]Ndipo Yesu akawaambia, "Mpeni
Kaisari kilicho cha Kaisari, naye Mungu
mpeni kilicho cha Mungu."
Nao wakamstaajabia sana.

*Ndoa Wakati Wa Ufufuo*

**(Mathayo 22:23-33; Luka 20:27-40)**

18 [h]Kisha Masadukayo, wale wasemao
kuwa hakuna ufufuo wa wafu, wakamjia
Yesu, 19 [i]wakasema, "Mwalimu, Mose
alituandikia kuwa kama ndugu wa mtu
akifa na kumwacha mkewe bila mtoto, basi
huyo mtu inampasa amwoe huyo mjane
ili amzalie ndugu yake watoto. 20 Basi
palikuwepo ndugu saba. Yule wa kwanza
akaoa mke, naye akafa pasipo kuwa na
mtoto yeyote. 21 Wa pili akamwoa yule
mjane, lakini naye akafa bila kuacha mtoto
yeyote. Ikawa vivyo hivyo kwa yule wa
tatu. 22 Hakuna hata mmojawapo wa hao
ndugu wote saba aliyeacha mtoto. Hatimaye
yule mwanamke naye akafa. 23 Kwa hiyo
wakati wa ufufuo, yeye atakuwa mke wa
nani, maana aliolewa na ndugu wote saba?"
24 [j]Yesu akawajibu, "Je, hampotoki kwa
sababu hamfahamu Maandiko wala uweza
wa Mungu? 25 [k]Wafu watakapofufuka,
hawataoa wala kuolewa, bali watakuwa
kama malaika wa mbinguni. 26 [l]Basi kuhusu
wafu kufufuliwa, je hamjasoma katika
Kitabu cha Mose jinsi Mungu alivyosema na
Mose kutoka kile kichaka akisema, 'Mimi ni
Mungu wa Abrahamu, na Mungu wa Isaki,
na Mungu wa Yakobo?' 27 Yeye si Mungu
wa wafu, bali ni Mungu wa walio hai. Kwa
hiyo mmekosea kabisa."

*Amri Iliyo Kuu*

**(Mathayo 22:34-40; Luka 10:25-28)**

28 [m]Mwalimu mmoja wa sheria akaja,
akawasikia wakijadiliana. Akiona kwamba

---

[a]**12:8** Ebr 13:12
[b]**12:10** Mdo 4:11
[c]**12:11** Za 119:22-23
[d]**12:12** Mk 11:18; Mt 22:22
[e]**12:13** Mt 22:16; Mk 3:6; Mt 12:10
[f]15 Dinari moja ilikuwa sawa na mshahara wa kibarua wa siku moja.
[g]**12:17** Rum 13:7
[h]**12:18** Mdo 4:1; 23:8; 1Kor 15:12
[i]**12:19** Kum 25:5
[j]**12:24** 2Tim 3:15-17
[k]**12:25** 1Kor 15:42, 49, 52
[l]**12:26** Kut 3:6
[m]**12:28** Lk 10:25-28; 20:39

Yesu amewajibu vyema, naye akamuuliza,
“Katika amri zote, ni ipi iliyo kuu?”
29 [a]Yesu akajibu, “Amri iliyo kuu ndiyo hii:
‘Sikia ee Israeli. Bwana Mungu wetu, Bwana
ndiye mmoja. 30 [b]Mpende Bwana Mungu
wako kwa moyo wako wote, kwa roho yako
yote, kwa akili zako zote, na kwa nguvu
zako zote.’ 31 [c]Ya pili ndiyo hii: ‘Mpende
jirani yako kama nafsi yako.’ Hakuna amri
nyingine iliyo kuu kuliko hizi.”
32 [d]Yule mwalimu wa sheria akamwambia
Yesu, “Mwalimu, umejibu vyema kwamba
Mungu ni mmoja, wala hakuna mwingine ila
yeye. 33 [e]Kumpenda Mungu kwa moyo wote
na kwa akili zote na kwa nguvu zote, na
kumpenda jirani kama mtu anavyojipenda
mwenyewe ni bora zaidi kuliko kutoa
sadaka za kuteketezwa na dhabihu zote.”
34 [f]Yesu alipoona kwamba amejibu kwa
busara, akamwambia, “Wewe hauko mbali
na Ufalme wa Mungu.” Tangu wakati huo,
hakuna mtu yeyote aliyethubutu kumuuliza
maswali tena.

*Kristo Ni Mwana Wa Nani?*

**(Mathayo 22:41-46; Luka 20:41-44)**

35 [g]Yesu alipokuwa akifundisha Hekaluni,
akauliza, “Imekuwaje walimu wa sheria
wanasema kwamba Kristo[h] ni Mwana wa
Daudi? 36 [i]Kwa maana Daudi mwenyewe,
akinena kwa kuongozwa na Roho Mtakatifu,
alisema:

“ ‘Bwana alimwambia Bwana wangu:
“Keti mkono wangu wa kuume,
hadi nitakapowaweka adui zako
chini ya miguu yako.” ’

37 [j]Kwa hiyo Daudi mwenyewe anamwita
‘Bwana.’ Awezaje basi yeye kuwa
mwanawe?”
Ule umati wote wa watu wakamsikiliza
kwa furaha.

*Yesu Awatahadharisha Watu Kuhusu Walimu Wa Sheria*

**(Mathayo 23:1-36; Luka 20:45-47)**

38 [k]Alipokuwa akifundisha, Yesu alisema,
“Jihadharini na walimu wa sheria. Wao
hupenda kutembea wakiwa wamevaa
mavazi marefu, na kusalimiwa kwa heshima
masokoni. 39 [l]Pia wao hupenda kukaa
kwenye viti vya mbele katika masinagogi,
na kupewa nafasi za heshima katika
karamu. 40 [m]Wao hula nyumba za wajane,
na ili waonekane kuwa wema wanasali sala
ndefu. Watu kama hawa watapata hukumu
iliyo kuu sana.”

*Sadaka Ya Mjane*

**(Luka 21:1-4)**

41 [n]Kisha Yesu akaketi mkabala na sehemu
ambapo sadaka zilikuwa zinawekwa na
kuangalia umati wa watu wakiweka fedha
zao kwenye sanduku la hazina ya Hekalu.
Matajiri wengi wakaweka kiasi kikubwa
cha fedha. 42 Lakini mjane mmoja maskini
akaja na kuweka sarafu mbili ndogo za
shaba zenye thamani ya senti mbili.
43 [o] Yesu akawaita wanafunzi wake,
akawaambia, “Amin, nawaambia, huyu
mjane maskini ameweka katika sanduku
la hazina zaidi ya watu wengine wote.
44 [p]Wengine wote wametoa kutokana na
ziada ya mali zao. Lakini huyu mjane
ametoa kutokana na umaskini wake,
akaweka kila kitu alichokuwa nacho, hata
kile alichohitaji ili kuishi.”

---

[a]**12:29** Kum 6:4; Lk 10:27
[b]**12:30** Kum 6:4-5
[c]**12:31** Law 19:18; Mt 5:43
[d]**12:32** Kum 4:35-39; Isa 46:9
[e]**12:33** Hes 6:6; Ebr 10:8
[f]**12:34** Mt 3:2; 22:46; Lk 20:40
[g]**12:35** Mt 26:55; 9:27
[h]35 *Kristo* maana yake ni *Masiya*, yaani *Aliyetiwa mafuta.*
[i]**12:36** 2Sam 23:2; Za 110:1; Mt 22:24
[j]**12:37** Yn 12:9
[k]**12:38** Mk 4:2; Mt 23:1; Lk 20:46; 11:43
[l]**12:39** Lk 11:43
[m]**12:40** Mt 23:14
[n]**12:41** 2Fal 12:9; Yn 8:20
[o]**12:43** 2Kor 8:12
[p]**12:44** 2Kor 8:12

*Dalili Za Siku Za Mwisho*

**(Mathayo 24:1-2; Luka 21:5-6)**

13 [a]Yesu alipokuwa akitoka Hekaluni,
mmojawapo wa wanafunzi wake
akamwambia, "Mwalimu! Tazama jinsi
mawe haya yalivyo makubwa, na majengo
haya yalivyo mazuri!"
2 [b]Ndipo Yesu akajibu akasema, "Je,
unayaona majengo haya yalivyo makubwa?
Hakuna hata jiwe moja litakalobaki juu ya
jingine, bali yote yatabomolewa."

*Mateso Yatabiriwa*

**(Mathayo 24:3-14; Luka 21:7-19)**

3 [c]Yesu alipokuwa ameketi kwenye Mlima
wa Mizeituni mkabala na Hekalu, Petro,
Yakobo, Yohana na Andrea wakamuuliza
faraghani, 4 [d]"Tafadhali tuambie, mambo
haya yatatukia lini? Nayo dalili ya kuwa
hayo yote yanakaribia kutimia itakuwa
gani?"
5 [e]Yesu akawaambia: "Jihadharini mtu
yeyote asiwadanganye. 6 Wengi watakuja
kwa Jina langu wakidai, 'Mimi ndiye,' nao
watawadanganya wengi. 7 Msikiapo habari
za vita na uvumi wa vita, msiwe na hofu.
Mambo haya hayana budi kutukia, lakini
ule mwisho bado. 8 [f]Taifa litainuka dhidi ya
taifa na ufalme dhidi ya ufalme. Kutakuwa
na mitetemeko sehemu mbalimbali na njaa.
Haya yatakuwa ndio mwanzo wa utungu.
9 [g]"Lakini ninyi jihadharini. Kwa maana
watawapeleka katika mabaraza yao na
kupigwa mijeledi katika masinagogi.
Mtashtakiwa mbele ya watawala na wafalme
kwa ajili yangu, ili kuwa ushuhuda kwao.
10 [h]Nayo habari njema lazima ihubiriwe
kwanza kwa mataifa yote kabla ule
mwisho haujawadia. 11 [i]Mtakapokamatwa
na kushtakiwa, msisumbuke awali kuhusu
mtakalosema. Semeni tu lolote mtakalopewa
wakati huo, kwa kuwa si ninyi mtakaokuwa
mkinena, bali ni Roho Mtakatifu.
12 [j]"Ndugu atamsaliti ndugu yake ili
auawe, naye baba atamsaliti mtoto wake.
Watoto nao wataasi dhidi ya wazazi wao
na kusababisha wauawe. 13 [k]Watu wote
watawachukia kwa ajili ya Jina langu.
Lakini yule atakayevumilia hadi mwisho
ataokolewa.

*Chukizo La Uharibifu*

**(Mathayo 24:15-28; Luka 21:20-24)**

14 [l]"Mtakapoona 'chukizo la uharibifu'
limesimama mahali pasipolipasa (asomaye
na afahamu), basi wale walioko Uyahudi
wakimbilie milimani. 15 Yeyote aliye juu ya
dari ya nyumba asishuke au kuingia ndani
ili kuchukua chochote. 16 Aliye shambani
asirudi nyumbani kuchukua vazi lake. 17 [m]Ole
wao wenye mimba na wale wanaonyonyesha
watoto siku hizo! 18 Ombeni mambo haya
yasitokee wakati wa baridi. 19 [n]Kwa maana
siku hizo zitakuwa za dhiki kuu ambayo
haijapata kuwako tangu mwanzo, hapo
Mungu alipoumba ulimwengu, mpaka
leo, na wala haitakuwako tena kamwe.
20 Kama Bwana asingelifupisha siku hizo,
kamwe asingeliokoka mtu yeyote. Lakini
kwa ajili ya wateule, wale aliowachagua,
amezifupisha siku hizo. 21 [o]Wakati huo mtu
yeyote akiwaambia, 'Tazama, Kristo[p] huyu
hapa!' au, 'Tazama, yuko kule,' msisadiki.
22 [q]Kwa maana watatokea makristo wa uongo
na manabii wa uongo, nao watafanya ishara
na maajabu ili kuwapotosha, ikiwezekana,
hata wale wateule. 23 [r]Hivyo jihadharini.
Nimekwisha kuwaambia mambo haya yote
mapema kabla hayajatukia.

---

[a]**13:1** Mt 24:1; Lk 21:5
[b]**13:2** Lk 19:44
[c]**13:3** Mt 21:1; 4:21
[d]**13:4** Mt 24:3; Lk 21:7
[e]**13:5** Yer 29:8; 1Tim 4:1
[f]**13:8** Mt 24:8; Isa 19:2; 2Nya 15:6
[g]**13:9** Mt 10:17
[h]**13:10** Mt 10:19-20
[i]**13:11** Lk 12:11-12
[j]**13:12** Mik 7:6; Lk 12:51-53
[k]**13:13** Yn 15:21; Mt 10:22
[l]**13:14** Dan 11:31; 12:11
[m]**13:17** Lk 22:39; 21:23
[n]**13:19** Mk 10:6; Dan 9:26; Yoe 2:2
[o]**13:21** Lk 17:23; 21:8
[p]21 *Kristo* maana yake ni *Masiya*, yaani *Aliyetiwa mafuta.*
[q]**13:22** Mt 7:15; Yn 4:48; 2The 2:9-10
[r]**13:23** 2Pet 3:17

*Kuja Kwa Mwana Wa Adamu*

**(Mathayo 24:29-31; Luka 21:25-28)**

24 [a]"Lakini katika siku hizo, baada ya hiyo
dhiki,

" 'jua litatiwa giza
nao mwezi hautatoa nuru yake;
25 [b]nazo nyota zitaanguka kutoka
angani,
na nguvu za anga zitatikisika.'

26 [c]"Ndipo watu wote watakapomwona
Mwana wa Adamu akija mawinguni
kwa nguvu nyingi na utukufu. 27 [d]Naye
atawatuma malaika wake wawakusanye
wateule wake kutoka pande zote nne za
dunia, kutoka miisho ya dunia hadi miisho
ya mbingu.

*Somo Kuhusu Mtini*

**(Mathayo 24:32-35; Luka 21:29-33)**

28 [e]"Basi jifunzeni somo hili kutokana na
mtini: Matawi yake yanapoanza kuchipua
na kutoa majani, mnatambua kwamba
wakati wa kiangazi umekaribia. 29 Vivyo
hivyo, myaonapo mambo haya yakitukia,
mnatambua kwamba wakati u karibu, hata
malangoni. 30 [f]Amin, nawaambia, kizazi hiki
hakitapita hadi mambo haya yote yawe
yametimia. 31 [g]Mbingu na nchi zitapita,
lakini maneno yangu hayatapita kamwe.

*Hakuna Ajuaye Siku Wala Saa*

**(Mathayo 24:36-44)**

32 [h]"Kwa habari ya siku ile na saa
hakuna yeyote ajuaye, hata malaika walio
mbinguni wala Mwana, ila Baba peke yake.
33 Jihadharini! Kesheni! Kwa maana hamjui
wakati ule utakapowadia. 34 [i]Ni kama mtu
anayesafiri. Anaiacha nyumba yake na
kuwaachia watumishi wake kuiangalia, kila
mtu na kazi yake, kisha akamwamuru yule
bawabu aliye mlangoni akeshe.
35 [j]"Basi kesheni kwa sababu hamjui ni
lini mwenye nyumba atakaporudi: iwapo
ni jioni, au ni usiku wa manane, au alfajiri
awikapo jogoo, au mapambazuko. 36 Kama
akija ghafula, asije akawakuta mmelala.
37 [k]Lile ninalowaambia ninyi, nawaambia
watu wote: 'Kesheni!' "

*Shauri La Kumuua Yesu*

**(Mathayo 26:1-5; Luka 22:1-2; Yohana 11:45-53)**

14 [l]Zilikuwa zimebaki siku mbili tu kabla
ya Sikukuu ya Pasaka, na Sikukuu ya
Mikate Isiyotiwa Chachu. Viongozi wa
makuhani na walimu wa sheria walikuwa
wakitafuta njia ya kumkamata Yesu kwa
hila na kumuua. 2 [m]Lakini walisema,
"Tusilifanye jambo hili wakati wa Sikukuu,
maana watu wanaweza wakafanya ghasia."

*Yesu Kupakwa Mafuta Huko Bethania*

**(Mathayo 26:6-13; Yohana 12:1-8)**

3 [n]Yesu alikuwa Bethania nyumbani
kwa Simoni aliyekuwa na ukoma. Wakati
alipokuwa ameketi mezani akila chakula
cha jioni, mwanamke mmoja aliingia akiwa
na chupa ya marhamu yenye manukato ya
nardo[o] safi ya thamani kubwa. Akaivunja
hiyo chupa, akamiminia hayo manukato
kichwani mwa Yesu.
4 Baadhi ya watu waliokuwepo pale
walikuwa wakisemezana wao kwa wao,
"Upotevu huu wote ni wa nini? 5 Mafuta
haya yangeweza kuuzwa kwa zaidi ya
dinari[p] 300, na fedha hizo wakapewa

---

[a]**13:24** Isa 13:10
[b]**13:25** Isa 34:4; Mt 24:9
[c]**13:26** Dan 7:13; Ufu 1:7
[d]**13:27** Zek 2:6
[e]**13:28** Mt 24:32; Lk 21:29
[f]**13:30** Lk 17:25; Mk 9:11
[g]**13:31** Mt 5:18
[h]**13:32** Mdo 1:7; 1The 5:1-2
[i]**13:34** Mt 25:14
[j]**13:35** Mt 24:42, 44
[k]**13:37** Lk 12:35-40
[l]**14:1** Yn 11:55; 13:1; Mt 12:14; 26:1-5; Lk 22:1-2
[m]**14:2** Mt 26:1-5; Lk 22:1-2
[n]**14:3** Mt 21:17; Lk 7:37-39
[o]3 Nardo ni aina ya manukato yaliyotengenezwa kutokana na mimea yenye mizizi inayotoa harufu nzuri.
[p]5 Dinari 300 ni sawa na mshahara wa kibarua wa siku 300.

maskini." Wakamkemea vikali huyo
mwanamke.
6 Lakini Yesu akawaambia, "Mbona
mnamsumbua huyu mwanamke?
Mwacheni! Yeye amenitendea jambo zuri
sana. 7 [a]Maskini mtakuwa nao siku zote
na mnaweza kuwasaidia wakati wowote
mnaotaka. Lakini mimi hamtakuwa nami
siku zote. 8 [b]Huyu mwanamke amenitendea
lile aliloweza. Ameumiminia mwili wangu
manukato ili kuniandaa kwa maziko
yangu. 9 [c]Amin, nawaambia, mahali popote
ulimwenguni ambapo Injili itahubiriwa,
jambo hili alilolitenda huyu mwanamke
litatajwa pia kwa ukumbusho wake."

*Yuda Akubali Kumsaliti Yesu*

**(Mathayo 26:14-16; Luka 22:3-6)**

10 [d]Kisha Yuda Iskariote, mmoja wa wale
wanafunzi kumi na wawili, akaenda kwa
viongozi wa makuhani ili kumsaliti Yesu
kwao. 11 [e]Walifurahi sana kusikia jambo
hili na wakaahidi kumpa fedha. Hivyo
yeye akawa anatafuta wakati uliofaa wa
kumsaliti.

*Yesu Ala Pasaka Na Wanafunzi Wake*

**(Mathayo 26:17-25; Luka 22:7-14, 21-23; Yohana 13:21-30)**

12 [fg]Siku ya kwanza ya Sikukuu ya Mikate
Isiyotiwa Chachu, siku ambayo kwa desturi
mwana-kondoo wa Pasaka huchinjwa,
wanafunzi wa Yesu wakamuuliza, "Unataka
twende wapi ili tukuandalie mahali pa kula
Pasaka?"
13 [h]Basi akawatuma wawili miongoni
mwa wanafunzi wake, akawaambia,
"Nendeni mjini. Huko mtakutana na
mwanaume amebeba mtungi wa maji.
Mfuateni. 14 [i]Mwambieni mwenye nyumba
ile atakayoingia, 'Mwalimu anauliza:
Kiko wapi chumba changu cha wageni,
ambamo mimi na wanafunzi wangu
tutakula Pasaka?' 15 [j]Atawaonyesha chumba
kikubwa ghorofani, kilichopambwa tena
kilicho tayari. Tuandalieni humo."
16 [k]Wale wanafunzi wakaondoka na
kwenda mjini, nao wakakuta kila kitu kama
Yesu alivyowaambia. Hivyo wakaiandaa
Pasaka.
17 [l]Ilipofika jioni, Yesu akaja pamoja
na wale wanafunzi wake kumi na wawili.
18 [m]Walipoketi mezani wakila, Yesu
akawaambia, "Amin, nawaambia, mmoja
wenu atanisaliti, mmoja anayekula pamoja
nami."
19 Wakaanza kuhuzunika na kumuuliza
mmoja baada ya mwingine, "Je, ni mimi
Bwana?"
20 [n]Akawajibu, "Ni mmoja miongoni
mwenu ninyi kumi na wawili, yule
anayechovya mkate kwenye bakuli pamoja
nami. 21 [o]Mwana wa Adamu anaenda zake
kama vile alivyoandikiwa. Lakini ole wake
mtu yule amsalitiye Mwana wa Adamu!
Ingekuwa heri kwake mtu huyo kama
hangezaliwa."

*Kuanzishwa Kwa Meza Ya Bwana*

**(Mathayo 26:26-30; Luka 22:14-20; 1 Wakorintho 11:23-25)**

22 [p]Walipokuwa wanakula, Yesu
akachukua mkate, akashukuru, akaumega
na kuwapa wanafunzi wake, akisema,
"Twaeni mle; huu ndio mwili wangu."
23 [q]Kisha akakitwaa kikombe, akashukuru,
akawapa, nao wote wakanywa kutoka
humo.
24 [r]Akawaambia, "Hii ndiyo damu yangu
ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi.

---

[a]**14:7** Kum 15:11
[b]**14:8** Yn 19:40
[c]**14:9** Mt 24:14; Mk 16:15
[d]**14:10** Mk 3:16-19; Mt 10:4; 26:14-16; Lk 23:3-6
[e]**14:11** Mt 26:14-16; Lk 22:3-6
[f]**14:12** Kum 16:1-4; 1Kor 5:7
[g]**14:12** Mt 26:17-19; 22:7-13
[h]**14:13** Mt 26:17-19; 22:7-13
[i]**14:14** Mt 26:17-19; 22:7-13
[j]**14:15** Mdo 1:13; Mt 26:17-19; 22:7-19
[k]**14:16** Mt 26:17-19; 22:7-19
[l]**14:17** Mt 26:20
[m]**14:18** Za 41:10
[n]**14:20** Yn 13:18-27
[o]**14:21** Mt 8:20
[p]**14:22** Mt 14:22
[q]**14:23** 1Kor 10:16
[r]**14:24** Mt 26:28

25 [a]Amin, nawaambia, sitakunywa tena
katika uzao wa mzabibu, hadi siku ile
nitakapounywa mpya katika Ufalme wa
Mungu."
26 [b]Walipokwisha kuimba wimbo,
wakatoka wakaenda Mlima wa Mizeituni.

*Yesu Atabiri Kuwa Petro Atamkana*

**(Mathayo 26:31-35; Luka 22:31-34; Yohana 13:36-38)**

27 [c]Yesu akawaambia, "Ninyi nyote
mtaniacha, kwa maana imeandikwa:

" 'Nitampiga mchungaji,
nao kondoo watatawanyika.'

28 [d]Lakini baada ya kufufuka kwangu,
nitawatangulia kwenda Galilaya."
29 [e]Petro akasema, "Hata kama wengine
wote watakuacha, mimi sitakuacha."
30 [f]Yesu akamwambia, "Amin, nakuambia;
leo, usiku huu, kabla jogoo hajawika mara
mbili, wewe mwenyewe utanikana mara
tatu."
31 [g]Lakini Petro akasisitiza zaidi, "Hata
kama itabidi kufa pamoja nawe, sitakukana
kamwe." Nao wale wengine wote wakasema
vivyo hivyo.

*Yesu Aomba Katika Bustani Ya Gethsemane*

**(Mathayo 26:36-46; Luka 22:39-46)**

32 [h]Wakaenda mahali paitwapo
Gethsemane. Yesu akawaambia wanafunzi
wake, "Kaeni hapa, nami niende nikaombe."
33 Kisha akawachukua pamoja naye Petro,
Yakobo na Yohana. Akaanza kuhuzunika
sana na kutaabika. 34 [i]Akawaambia, "Moyo
wangu umejawa na huzuni kiasi cha kufa.
Kaeni hapa na mkeshe."
35 [j]Akaenda mbele kidogo, akaanguka
kifudifudi, akaomba kwamba kama
ingewezekana saa hiyo ya mateso
imwondokee. 36 [k]Akasema, "*Abba,*[l] Baba,
mambo yote yawezekana kwako. Niondolee
kikombe hiki. Lakini si kama nipendavyo
mimi, bali vile upendavyo wewe."
37 Akarudi kwa wanafunzi wake,
akawakuta wamelala. Akamwambia Petro,
"Simoni, umelala? Je, hukuweza kukesha
hata kwa saa moja? 38 [m]Kesheni na mwombe,
msije mkaingia majaribuni. Roho iko radhi,
lakini mwili ni mdhaifu."
39 Akaenda tena kuomba, akisema maneno
yale yale. 40 Aliporudi, akawakuta tena
wamelala kwa sababu macho yao yalikuwa
mazito. Nao hawakujua la kumwambia.
41 [n]Akaja mara ya tatu, akawaambia,
"Bado mmelala na kupumzika? Imetosha!
Saa imewadia. Tazameni, Mwana wa
Adamu anasalitiwa na kutiwa mikononi
mwa wenye dhambi. 42 [o]Inukeni, twende
zetu! Tazameni, msaliti wangu yuaja!"

*Yesu Akamatwa*

**(Mathayo 26:47-56; Luka 22:47-53; Yohana 18:3-12)**

43 [p]Yesu alipokuwa bado anazungumza,
Yuda, mmoja wa wale wanafunzi Kumi na
Wawili, akatokea. Alikuwa amefuatana na
umati wa watu wenye panga na marungu,
waliokuwa wametumwa na viongozi wa
makuhani, walimu wa sheria, na wazee.
44 Basi msaliti alikuwa amewapa hao
watu ishara, kwamba: "Yule nitakayembusu
ndiye. Mkamateni, mkamchukue chini ya
ulinzi." 45 [q]Mara Yuda akamjia Yesu na

---

[a]**14:25** Mt 3:2
[b]**14:26** Mt 21:1
[c]**14:27** Zek 13:7
[d]**14:28** Mk 16:7
[e]**14:29** Mt 26:33-34; Lk 22:33, 34; Yn 13:37, 38
[f]**14:30** Lk 22:34; Yn 13:38
[g]**14:31** Lk 22:33; Yn 13:37
[h]**14:32** Mt 26:36; Lk 22:29; Yn 13:37
[i]**14:34** Yn 12:27
[j]**14:35** Mk 14:41; Mt 26:18
[k]**14:36** Rum 8:15; Gal 4:6; Mt 20:22; 26:39
[l]36 *Abba* ni neno la Kiaramu ambalo maana yake ni *Baba*
[m]**14:38** Mt 6:13; Rum 7:22-23
[n]**14:41** Mt 26:18
[o]**14:42** Mt 26:46; Yn 18:1, 2
[p]**14:43** Mt 10:4
[q]**14:45** Mt 23:7

kusema, “Rabi.”[a] Akambusu. 46 Wale watu
wakamkamata Yesu, wakamweka chini ya
ulinzi. 47 Ndipo mmoja wa wale waliokuwa
wamesimama karibu aliuchomoa upanga
wake na kumpiga mtumishi wa kuhani
mkuu, akamkata sikio.

48 [b]Kisha Yesu akawaambia, “Mmekuja
na panga na marungu kunikamata kana
kwamba mimi ni mnyang’anyi? 49 [c]Siku kwa
siku nilikuwa pamoja nanyi nikifundisha
Hekaluni, wala hamkunikamata. Lakini
Maandiko sharti yatimie.” 50 [d]Ndipo
wanafunzi wake wote wakamwacha,
wakakimbia.

51 Kijana mmoja, ambaye hakuwa amevaa
kitu isipokuwa alijitanda nguo ya kitani,
alikuwa akimfuata Yesu. Walipomkamata,
52 alikimbia uchi, akaliacha vazi lake.

*Yesu Mbele Ya Baraza La Wayahudi*

### (Mathayo 26:57-68; Luka 22:54-71; Yohana 18:13-24)

53 [e]Wakampeleka Yesu kwa kuhani mkuu,
nao viongozi wa makuhani wote, na wazee
na walimu wa sheria wote wakakusanyika
pamoja. 54 [f]Petro akamfuata kwa mbali,
hadi uani kwa kuhani mkuu. Huko akaketi
pamoja na walinzi, akiota moto.

55 [g]Viongozi wa makuhani na Baraza
la Wayahudi[h] lote wakatafuta ushahidi
dhidi ya Yesu ili wapate kumuua. Lakini
hawakupata jambo lolote. 56 Wengi walitoa
ushahidi wa uongo dhidi yake, lakini
maelezo yao hayakukubaliana.

57 Ndipo wengine wakasimama
wakatoa ushahidi wa uongo dhidi yake,
wakisema: 58 [i]“Sisi tulimsikia akisema,
‘Mimi nitalibomoa Hekalu hili lililojengwa
na wanadamu, na katika siku tatu
nitajenga jingine ambalo halikujengwa na
wanadamu.’ ” 59 Lakini hata hivyo, ushahidi
wao haukukubaliana.

60 [j]Basi kuhani mkuu akasimama mbele
yao, akamuuliza Yesu, “Je, wewe hutajibu?
Ni ushahidi gani hawa watu wanauleta
dhidi yako?” 61 [k]Lakini Yesu akakaa kimya,
hakusema neno lolote.

Kuhani mkuu akamuuliza tena, “Je,
wewe ndiwe Kristo,[l] Mwana wa Mungu
Aliyebarikiwa?”

62 [m]Yesu akajibu, “Mimi ndimi. Nanyi
mtamwona Mwana wa Adamu akiwa
ameketi mkono wa kuume wa Mwenye
Nguvu, na akija juu ya mawingu ya
mbinguni.”

63 [n]Kuhani mkuu akararua mavazi yake,
akasema, “Tuna haja gani tena ya mashahidi
zaidi? 64 [o]Ninyi mmesikia hayo makufuru.
Uamuzi wenu ni gani?”

Wote wakamhukumu kwamba
anastahili kifo. 65 [p]Kisha baadhi ya watu
wakaanza kumtemea mate; wakamfunga
kitambaa machoni, wakampiga kwa
ngumi na kumwambia, “Tabiri!” Walinzi
wakamchukua na kumpiga makofi.

*Petro Amkana Yesu*

### (Mathayo 26:69-75; Luka 22:56-62; Yohana 18:15-18, 25-27)

66 [q]Petro alipokuwa bado yuko chini
kwenye ua wa jumba la kifalme, tazama
akaja mmoja wa watumishi wa kike wa

---

[a]45 *Rabi* ni neno la Kiebrania ambalo maana yake ni daktari, mwalimu au bwana. Walikuwa na madaraja matatu: La chini kabisa *Rab* (bwana), la pili *Rabi* (bwana wangu), na la juu kabisa *Raboni* (mkuu wangu, bwana wangu mkuu).
[b]**14:48** Mt 26:55; Lk 22:52
[c]**14:49** Mt 26:55; Isa 53:7-12
[d]**14:50** Za 88:8; Mk 14:27
[e]**14:53** Mt 26:57; Yn 18:13
[f]**14:54** Mt 26:3; Yn 18:18
[g]**14:55** Mt 5:22
[h]55 *Baraza la Wayahudi* hapa ina maana ya *Sanhedrin* ambalo lilikuwa ndilo baraza la juu kabisa la utawala wa Kiyahudi, lililoundwa na wazee 70 pamoja na kuhani mkuu.
[i]**14:58** Mk 15:29; Yn 2:19
[j]**14:60** Mt 26:62
[k]**14:61** Isa 54:7; Lk 23:9; Mt 16:16; Yn 4:25-26
[l]61 *Kristo* maana yake ni *Masiya*, yaani *Aliyetiwa mafuta.*
[m]**14:62** Ufu 1:7; Dan 7:13
[n]**14:63** Hes 14:6; Mdo 14:14
[o]**14:64** Law 24:16
[p]**14:65** Mt 16:21
[q]**14:66** Lk 22:55; Yn 18:16

kuhani mkuu. 67 [a]Alipomwona Petro akiota
moto, akamtazama sana, akamwambia,
“Wewe pia ulikuwa pamoja na Yesu,
Mnazareti.”
68 [b]Lakini Petro akakana, akasema, “Sijui
wala sielewi unalosema.” Naye akaondoka
kuelekea kwenye njia ya kuingilia.
69 [c]Yule mtumishi wa kike alipomwona
mahali pale, akawaambia tena wale
waliokuwa wamesimama hapo, “Huyu mtu
ni mmoja wao.” 70 [d]Lakini Petro akakana
tena.
Baada ya muda kidogo wale waliokuwa
wamesimama hapo karibu na Petro
wakamwambia, “Hakika wewe ni mmoja
wao, kwa maana wewe pia ni Mgalilaya!”
71 [e]Petro akaanza kujilaani na kuwaapia,
“Mimi simjui huyu mtu mnayesema habari
zake!”
72 [f]Papo hapo jogoo akawika mara ya
pili. Ndipo Petro akakumbuka lile neno
Yesu alikuwa amemwambia: “Kabla jogoo
hajawika mara mbili, utanikana mara tatu.”
Akavunjika moyo, akalia sana.

*Yesu Mbele Ya Pilato*

**(Mathayo 27:1-14; Luka 23:1-5; Yohana 18:28-38)**

15 [g]Asubuhi na mapema, viongozi wa
makuhani, pamoja na wazee, walimu
wa sheria na Baraza lote, wakafikia uamuzi.
Wakamfunga Yesu, wakamchukua na
kumkabidhi kwa Pilato.
2 [h]Pilato akamuuliza, “Je, wewe ndiye
Mfalme wa Wayahudi?”
Yesu akajibu, “Wewe umesema.”
3 Viongozi wa makuhani wakamshtaki
kwa mambo mengi. 4 [i]Pilato akamuuliza
tena, “Je, huna la kujibu? Tazama ni
mashtaka mangapi wanayaleta juu yako.”
5 [j]Lakini Yesu hakujibu lolote, hivyo
Pilato akashangaa.

*Pilato Amtoa Yesu Asulubiwe*

**(Mathayo 27:15-26; Luka 23:13-25; Yohana 18:39–19:16)**

6 [k]Ilikuwa desturi wakati wa Sikukuu
ya Pasaka kumfungulia mfungwa yeyote
ambaye watu wangemtaka. 7 Wakati huo,
mtu aliyeitwa Baraba alikuwa amefungwa
gerezani pamoja na waasi wengine
waliokuwa wametekeleza uuaji wakati wa
maasi. 8 Ule umati wa watu ukamjia Pilato
na kumwomba awafanyie kama ilivyokuwa
desturi yake.
9 Pilato akawauliza, “Mnataka
niwafungulie huyu Mfalme wa Wayahudi?”
10 [l]Kwa maana yeye alitambua kuwa
viongozi wa makuhani walikuwa wamemtia
Yesu mikononi mwake kwa ajili ya
wivu. 11 [m]Lakini viongozi wa makuhani
wakauchochea ule umati wa watu
wamwombe awafungulie Baraba badala
yake.
12 Pilato akawauliza tena, “Basi mnataka
nifanye nini na huyu mtu mnayemwita
Mfalme wa Wayahudi?”
13 Wakapiga kelele wakisema,
“Msulubishe!”
14 Pilato akawauliza, “Kwa nini?
Amefanya kosa gani?”
Lakini wao wakapiga kelele kwa nguvu
zaidi, wakisema, “Msulubishe!”
15 [n]Pilato, akitaka kuuridhisha ule umati
wa watu, akawafungulia Baraba. Naye
baada ya kuamuru Yesu achapwe mijeledi,
akamtoa ili asulubishwe.

*Askari Wamdhihaki Yesu*

**(Mathayo 27:27-31; Yohana 19:2-3)**

16 [o]Askari wakampeleka Yesu hadi
kwenye ukumbi wa ndani wa jumba la

[a]**14:67** Mk 14:54; 1:24
[b]**14:68** Mk 14:30, 72
[c]**14:69** Mt 26:71; Lk 22:58; Yn 18:25
[d]**14:70** Mdo 2:7
[e]**14:71** Mk 14:30, 72
[f]**14:72** Mk 14:30, 68; Mt 26:75; Mk 14:50
[g]**15:1** Mt 27:1-2; Lk 22:66; Mt 5:22
[h]**15:2** Mt 2:2
[i]**15:4** Mt 27:13
[j]**15:5** Mk 14:61
[k]**15:6** Mt 27:15; Lk 23:17; Yn 18:39
[l]**15:10** Yn 11:48; 12:19; Mt 27:38
[m]**15:11** Mdo 3:14
[n]**15:15** Isa 53:6; Mt 27:26; Yn 19:1, 36
[o]**15:16** Yn 18:28-33; 19:9

kifalme, ndio Praitorio,[a] wakakusanya kikosi kizima cha askari. 17 Wakamvalisha Yesu joho la zambarau, wakasokota taji ya miiba, wakamvika kichwani. 18 Wakaanza kumsalimu kwa dhihaka, "Salamu, mfalme wa Wayahudi!" 19 Wakampiga kwa fimbo ya mwanzi tena na tena kichwani na kumtemea mate. Wakapiga magoti mbele yake, wakamsujudia kwa kumdhihaki. 20 [b]Walipokwisha kumdhihaki, wakamvua lile joho la zambarau, wakamvika tena nguo zake. Kisha wakamtoa nje ili wakamsulubishe.

*Kusulubiwa Kwa Yesu*

**(Mathayo 27:32-44; Luka 23:26-43; Yohana 19:17-27)**

21 [c]Mtu mmoja kutoka Kirene, jina lake Simoni, baba yao Aleksanda na Rufo, alikuwa anapita zake kuingia mjini kutoka shamba, nao wakamlazimisha kuubeba ule msalaba. 22 [d]Kisha wakampeleka Yesu mpaka mahali palipoitwa Golgotha (maana yake ni Mahali pa Fuvu la Kichwa). 23 [e]Nao wakampa divai iliyochanganywa na manemane, lakini hakuinywa. 24 [f]Basi wakamsulubisha, nazo nguo zake wakagawana miongoni mwao kwa kuzipigia kura ili kuamua ni gani kila mtu ataichukua.

25 [g]Ilikuwa yapata saa tatu asubuhi walipomsulubisha. 26 [h]Tangazo likaandikwa la mashtaka dhidi yake lenye maneno haya: "MFALME WA WAYAHUDI." 27 [i]Pamoja naye walisulubiwa wanyang'anyi wawili, mmoja upande wake wa kuume na mwingine upande wa kushoto. [ 28 [j]Nayo maandiko yakatimizwa, yale yasemayo, "Alihesabiwa pamoja na watenda dhambi.]" 29 [k]Watu waliokuwa wakipita njiani wakamtukana huku wakitikisa vichwa vyao na kusema, "Aha! Wewe ambaye utalivunja Hekalu na kulijenga kwa siku tatu, 30 basi shuka kutoka msalabani na ujiokoe mwenyewe!"

31 [l]Vivyo hivyo, viongozi wa makuhani pamoja na walimu wa sheria wakamdhihaki miongoni mwao wakisema, "Aliwaokoa wengine, lakini hawezi kujiokoa mwenyewe! 32 [m]Basi huyu Kristo,[n] huyu Mfalme wa Israeli, ashuke sasa kutoka msalabani, ili tupate kuona na kuamini." Wale waliosulubiwa pamoja naye pia wakamtukana.

*Kifo Cha Yesu Msalabani*

**(Mathayo 27:45-56; Luka 23:44-49; Yohana 19:28-30)**

33 [o]Ilipofika saa sita, giza liliifunika nchi yote hadi saa tisa. 34 [p]Mnamo saa tisa, Yesu akapaza sauti, akalia, *"Eloi, Eloi, lama sabakthani?"* (maana yake, "Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?")

35 Baadhi ya watu waliokuwa wamesimama karibu waliposikia hayo, wakasema, "Msikieni, anamwita Eliya."

36 [q]Mtu mmoja akaenda mbio, akachovya sifongo kwenye siki, akaiweka kwenye mwanzi na akampa Yesu ili anywe, akisema, "Basi mwacheni. Hebu tuone kama Eliya atakuja kumshusha kutoka hapo msalabani."

37 [r]Kisha Yesu akatoa sauti kuu, akakata roho.

38 [s]Pazia la Hekalu likachanika vipande viwili kuanzia juu hadi chini. 39 [t]Basi yule jemadari aliyekuwa amesimama hapo mbele ya msalaba wa Yesu aliposikia ile

[a]16 Praitorio maana yake ni makao makuu ya mtawala; ni jumba la kifalme lililokuwa linakaliwa na Pontio Pilato huko Yerusalemu, palipokuwa na kiti cha hukumu.
[b]**15:20** Ebr 13:12
[c]**15:21** Mt 27:32; Lk 23:36
[d]**15:22** Mt 27:33; Lk 23:33; Yn 19:17
[e]**15:23** Za 69:21; Mit 31:6
[f]**15:24** Za 22; 18
[g]**15:25** Mt 27:45; Lk 23:44; Yn 19:14
[h]**15:26** Mt 27:37; Yn 19:19; Mk 15:2
[i]**15:27** Mt 27:38
[j]**15:28** Isa 51:12; Lk 22:37
[k]**15:29** Za 22:7; 109:25; Mk 14:58; Yn 2:19
[l]**15:31** Za 22:7
[m]**15:32** Mk 14:61; 15:2
[n]32 *Kristo* maana yake ni *Masiya*, yaani *Aliyetiwa mafuta.*
[o]**15:33** Amo 8:9
[p]**15:34** Za 21:1; Mt 27:46
[q]**15:36** Mk 15:23; Za 69:21
[r]**15:37** Yn 19:30
[s]**15:38** Ebr 10:19-20
[t]**15:39** Mt 4:3; Mk 9:7

sauti yake na kuona jinsi alivyokata roho,
akasema, “Hakika mtu huyu alikuwa
Mwana wa Mungu!”
40 [a]Walikuwepo pia wanawake waliokuwa
wakiangalia kwa mbali. Miongoni mwao
walikuwepo Maria Magdalene, na Maria
mama yao Yakobo mdogo na Yose, pia na
Salome. 41 [b]Hawa walifuatana na Yesu na
kushughulikia mahitaji yake alipokuwa
Galilaya. Pia walikuwepo wanawake
wengine wengi waliokuwa wamekuja
pamoja naye Yerusalemu.

*Maziko Ya Yesu*

**(Mathayo 27:57-61; Luka 23:50-56; Yohana 19:38-42)**

42 [c]Ilipofika jioni, kwa kuwa ilikuwa
Siku ya Maandalizi, yaani siku moja kabla
ya Sabato, 43 [d]Yosefu wa Arimathaya,
mtu aliyeheshimiwa katika Baraza, na
ambaye alikuwa anautarajia Ufalme wa
Mungu, akamwendea Pilato kwa ujasiri
na kumwomba mwili wa Yesu. 44 Pilato
alikuwa akijiuliza kama Yesu alikuwa
amekwisha kufa. Hivyo akamwita yule
jemadari, akamuuliza iwapo Yesu alikuwa
amekwisha kufa. 45 [e]Baada ya kupata habari
kutoka kwa yule jemadari kwamba kweli
amekwisha kufa, Pilato akampa Yosefu
ruhusa ya kuuchukua huo mwili. 46 [f]Hivyo
Yosefu akanunua kitambaa cha kitani
safi, akaushusha mwili kutoka msalabani,
akaufunga katika kile kitambaa cha kitani,
na kuuweka ndani ya kaburi lililochongwa
kwenye mwamba. Kisha akavingirisha jiwe
kwenye ingilio la kaburi. 47 Maria Magdalene
na Maria mamaye Yose walipaona mahali
pale alipolazwa.

[a]**15:40** Za 38:11; Lk 24:10; Yn 19:25
[b]**15:41** Mt 27:55-56; Lk 8:2-3
[c]**15:42** Mt 27:62; Yn 19:31
[d]**15:43** Mt 5:22; 3:2; Lk 2:25, 38
[e]**15:45** Mk 15:39
[f]**15:46** Mk 16:3

*Kufufuka Kwa Yesu*

**(Mathayo 28:1-8; Luka 24:1-12; Yohana 20:1-10)**

16 [g]Sabato ilipomalizika, Maria
Magdalene, Maria mama yake
Yakobo, na Salome walinunua manukato
ili wakaupake mwili wa Yesu. 2 [h]Asubuhi
na mapema, siku ya kwanza ya juma, mara
tu baada ya kuchomoza jua, walikwenda
kaburini. 3 [i]Njiani wakawa wanaulizana wao
kwa wao, “Ni nani atakayetuvingirishia lile
jiwe kutoka kwenye ingilio la kaburi?”
4 Lakini walipotazama, wakaona lile jiwe,
ambalo lilikuwa kubwa sana, limekwisha
kuvingirishwa kutoka pale penye ingilio
la kaburi. 5 [j]Walipokuwa wakiingia mle
kaburini, wakamwona kijana mmoja
aliyevaa joho jeupe akiwa ameketi upande
wa kuume, nao wakastaajabu.
6 [k]Yule malaika akawaambia,
“Msistaajabu. Mnamtafuta Yesu, Mnazareti,
aliyesulubiwa. Amefufuka! Hayuko hapa.
Tazameni mahali walipomlaza. 7 [l]Lakini
nendeni mkawaambie wanafunzi wake
pamoja na Petro, kwamba, ‘Anawatangulia
kwenda Galilaya. Huko ndiko mtamwona,
kama alivyowaambia.’ ”
8 [m]Hivyo wakatoka, wakakimbia kutoka
mle kaburini wakiwa na hofu kuu na
mshangao. Nao hawakumwambia mtu
yeyote neno lolote, kwa sababu waliogopa.

*Yesu Anamtokea Maria Magdalene*

**(Mathayo 28:9-10; Yohana 20:11-18)**

9 [n]Yesu alipofufuka alfajiri na mapema
siku ya kwanza ya juma alimtokea
kwanza Maria Magdalene, yule ambaye
alikuwa amemtoa pepo wachafu saba.
10 [o]Maria akaenda, naye akawaambia
wale waliokuwa wamefuatana na Yesu,

[g]**16:1** Lk 24:9; Yn 19:39-40
[h]**16:2** Lk 24:1; Yn 20:1
[i]**16:3** Mk 15:46
[j]**16:5** Lk 24:3-4
[k]**16:6** Mk 1:24
[l]**16:7** Yn 21:1-23; Mk 14:28
[m]**16:8** Mt 28:8; Lk 24:9
[n]**16:9** Mk 15:4-7
[o]**16:10** Lk 24:10; Yn 20:18

waliokuwa wanaomboleza na kulia.
11 [a]Lakini waliposikia kwamba Yesu yu hai
na kwamba Maria alikuwa amemwona,
hawakusadiki.

*Yesu Awatokea Wanafunzi Wawili*

**(Luka 24:13-35)**

12 [b]Baadaye Yesu akawatokea wawili
miongoni mwa wanafunzi wake walipokuwa
wakienda shambani akiwa katika sura
nyingine. 13 Nao wakarudi na kuwaambia
wenzao. Lakini hawakuwasadiki wao pia.

*Yesu Awaagiza Wale Wanafunzi Kumi Na Mmoja*

**(Mathayo 28:16-20; Luka 24:36-49; Yohana 20:19-23; Matendo 1:6-8)**

14 [c]Baadaye Yesu akawatokea wale
wanafunzi kumi na mmoja walipokuwa
wakila chakula. Akawakemea kwa
kutoamini kwao na kwa ugumu wa mioyo
yao kwa kutosadiki wale waliomwona
baada yake kufufuka.
15 [d]Akawaambia, “Enendeni ulimwenguni
kote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.
16 [e]Yeyote aaminiye na kubatizwa ataokoka.
Lakini yeyote asiyeamini atahukumiwa.
17 [f]Nazo ishara hizi zitafuatana na
wanaoamini: Kwa Jina langu watatoa
pepo wachafu; watasema kwa lugha mpya;
18 [g]watashika nyoka kwa mikono yao; na
hata wakinywa kitu chochote cha kuua,
hakitawadhuru kamwe; wataweka mikono
yao juu ya wagonjwa, nao watapona.”

*[Yesu Apaa Kwenda Mbinguni*

**(Luka 24:50-53; Matendo 1:9-11)**

19 [h]Baada ya Bwana Yesu kusema nao,
alichukuliwa juu mbinguni na kuketi
mkono wa kuume wa Mungu. 20 [i]Kisha
wanafunzi wake wakatoka, wakahubiri kila
mahali, naye Bwana akatenda kazi pamoja
nao na kulithibitisha neno lake kwa ishara
zilizofuatana nalo.]

[a]**16:11** Mk 16:13, 14; Lk 24:11
[b]**16:12** Lk 24:13-32
[c]**16:14** Lk 24:36-43
[d]**16:15** Mt 28:18-20; Mdo 1:8
[e]**16:16** Mdo 16:31; Yn 12:48
[f]**16:17** Lk 10:17; 1Kor 13:1; 14:2-39
[g]**16:18** Lk 10:19; Mdo 28:3-5; 6:6
[h]**16:19** Lk 24:50-51; Yn 6:6; Mdo 1:19; 1Tim 3:16; Za 110:1; Mt 26:64; Mdo 2:33; 5:31; Rum 8:34; Kol 3:1; Ebr 1:3; 12:2
[i]**16:20** Yn 4:48

# LUKA

1 Kwa kuwa watu wengi wamekaa ili
kuandika habari za mambo yaliyotukia
katikati yetu, 2 [a]kama vile yalivyokabidhiwa
kwetu na wale waliokuwa mashahidi
walioyaona na watumishi wa Bwana,
3 [b]mimi nami baada ya kuchunguza kila kitu
kwa uangalifu kuanzia mwanzo, niliamua
kukuandikia habari za mambo hayo, ewe
mtukufu Theofilo, 4 [c]ili upate kujua ukweli
kuhusu yale uliyofundishwa.

*Kuzaliwa Kwa Yohana Mbatizaji Kwatabiriwa*

5 [d]Wakati wa Herode mfalme wa
Uyahudi, palikuwa na kuhani mmoja jina
lake Zekaria, ambaye alikuwa wa ukoo
wa kikuhani wa Abiya. Elizabeti mkewe
alikuwa pia mzao wa Aroni. 6 [e]Zekaria
na Elizabeti mkewe wote walikuwa watu
wanyofu mbele za Mungu, wakizishika
amri zote za Bwana na maagizo yote bila
lawama. 7 Lakini walikuwa hawana watoto,
kwa sababu Elizabeti alikuwa tasa; nao
wote wawili walikuwa wazee sana.

8 [f]Siku moja ilipokuwa zamu ya kikundi
cha Zekaria, yeye akifanya kazi ya ukuhani
Hekaluni mbele za Mungu, 9 [g]alichaguliwa
kwa kura kwa kufuata desturi za ukuhani,
kuingia Hekaluni mwa Bwana ili kufukiza
uvumba. 10 [h]Nao wakati wa kufukiza
uvumba ulipowadia, wale wote waliokuwa
wamekusanyika ili kuabudu walikuwa nje
wakiomba.

11 [i]Ndipo malaika wa Bwana, akiwa
amesimama upande wa kuume wa
madhabahu ya kufukizia uvumba,
akamtokea Zekaria. 12 [j]Zekaria alipomwona
huyo malaika, akafadhaika sana, akajawa
na hofu. 13 [k]Lakini malaika akamwambia,
“Usiogope, Zekaria, kwa maana Mungu
amesikia maombi yako. Mkeo Elizabeti
atakuzalia mtoto wa kiume, nawe utamwita
jina lake Yohana. 14 [l]Yeye atakuwa furaha
na shangwe kwako, nao watu wengi
watashangilia kwa sababu ya kuzaliwa
kwake. 15 [m]Kwa kuwa atakuwa mkuu
mbele za Bwana, kamwe hataonja mvinyo
wala kinywaji chochote cha kulevya, naye
atajazwa Roho Mtakatifu hata kabla ya
kuzaliwa kwake. 16 [n]Naye atawageuza wengi
wa wana wa Israeli warudi kwa Bwana
Mungu wao. 17 [o]Naye atatangulia mbele
za Bwana katika roho na nguvu ya Eliya,
ili kuigeuza mioyo ya baba kuwaelekea
watoto wao, na wasiotii warejee katika
hekima ya wenye haki, ili kuliweka tayari
taifa lililoandaliwa kwa ajili ya Bwana.”

18 [p]Zekaria akamuuliza malaika, “Jambo
hilo linawezekanaje? Mimi ni mzee na mke
wangu pia ana umri mkubwa.”

19 [q]Malaika akamjibu, akamwambia,
“Mimi ni Gabrieli, nisimamaye mbele
za Mungu, nami nimetumwa kwako ili
nikuambie habari hizi njema. 20 [r]Basi
sasa kwa kuwa hujaamini maneno yangu
ambayo yatatimizwa kwa wakati wake,
utakuwa bubu hadi siku ile mambo haya
yatakapotukia.”

21 Wakati huo watu walikuwa
wanamngojea Zekaria nje huku
wakishangaa kukawia kwake mle Hekaluni.
22 [s]Alipotoka akawa hawezi kusema nao,
wao wakatambua kuwa ameona maono
ndani ya Hekalu. Lakini kwa kuwa alikuwa
bubu, akawa anawaashiria kwa mikono.

[a]**1:2** Mk 1:1; Mdo 1:21-22; 2Pet 1:16; 1Yn 1:1; Mk 4:14
[b]**1:3** Mdo 11:4; 24:3; 26:25; 1:1
[c]**1:4** Yn 20:31; Mdo 2:42
[d]**1:5** 1Nya 24:10; Mt 2:1
[e]**1:6** Kum 5:33; Lk 2:25
[f]**1:8** 1Nya 24:19; 2Nya 8:14
[g]**1:9** 2Nya 29:11; Za 141:2
[h]**1:10** Law 16:17
[i]**1:11** Mdo 5:19; Kut 30:1-10
[j]**1:12** Amu 6:22-23; 13:22
[k]**1:13** Mt 14:27; 3:1; Lk 1:60-63
[l]**1:14** Lk 1:58
[m]**1:15** Law 10:9; Lk 7:33; Yer 1:5; Gal 1:15
[n]**1:16** Mal 4:5, 6
[o]**1:17** Mt 11:14; Mal 4:4-6
[p]**1:18** Mwa 17:17
[q]**1:19** Mt 18:10; Lk 1:26
[r]**1:20** Kut 4:11; Eze 3:26
[s]**1:22** Lk 1:62

23 [a]Muda wake wa kuhudumu Hekaluni ulipomalizika, akarudi nyumbani kwake. 24 Baada ya muda usio mrefu, Elizabeti mkewe akapata mimba, naye akajitenga kwa miezi mitano.

25 [b]Akasema, "Hili ndilo Bwana alilonitendea aliponiangalia kwa upendeleo na kuniondolea aibu yangu mbele ya watu."

*Kuzaliwa Kwa Yesu Kwatabiriwa*

26 [c]Mwezi wa sita baada ya Elizabeti kupata mimba, Mungu alimtuma malaika Gabrieli aende Galilaya katika mji wa Nazareti, 27 [d]kwa mwanamwali bikira aliyekuwa ameposwa na mtu mmoja jina lake Yosefu wa nyumba ya Daudi. Jina la huyu mwanamwali bikira ni Maria. 28 [e]Naye malaika akaja kwake akamwambia: "Salamu, wewe uliyebarikiwa, Bwana yu pamoja nawe!"

29 [f]Maria akafadhaishwa sana na maneno haya, akajiuliza moyoni, "Salamu hii ni ya namna gani?" 30 [g]Ndipo malaika akamwambia, "Usiogope, Maria, umepata kibali kwa Mungu. 31 [h]Tazama, utachukua mimba, nawe utamzaa mtoto mwanaume na utamwita jina lake Yesu. 32 [i]Yeye atakuwa mkuu, naye ataitwa Mwana wa Aliye Juu Sana. BWANA Mungu atampa kiti cha enzi cha Daudi baba yake. 33 [j]Ataimiliki nyumba ya Yakobo milele, na ufalme wake hautakuwa na mwisho."

34 Maria akamuuliza huyo malaika, "Maadamu mimi ni bikira, jambo hili litawezekanaje?"

35 [k]Malaika akamjibu, "Roho Mtakatifu atakujilia juu yako, nazo nguvu zake Yeye Aliye Juu Sana zitakufunika kama kivuli. Kwa hiyo mtoto atakayezaliwa atakuwa mtakatifu, naye ataitwa Mwana wa Mungu. 36 [l]Tazama, jamaa yako Elizabeti amechukua mimba katika uzee wake, na huu ni mwezi wake wa sita, yeye aliyeitwa tasa. 37 [m]Kwa maana kwa Mungu hakuna lisilowezekana."

38 Maria akasema, "Tazama, mimi ni mtumishi wa Bwana. Na iwe kwangu kama ulivyosema." Kisha malaika akaondoka, akamwacha.

*Maria Aenda Kumtembelea Elizabeti*

39 [n]Wakati huo Maria akajiandaa, akaharakisha kwenda katika mji mmoja kwenye vilima vya Uyahudi. 40 Akaingia nyumbani kwa Zekaria na kumsalimu Elizabeti. 41 [o]Naye Elizabeti aliposikia salamu ya Maria, mtoto aliyekuwa tumboni mwake akaruka. Elizabeti akajazwa na Roho Mtakatifu, 42 [p]akapaza sauti kwa nguvu akasema, "Umebarikiwa wewe miongoni mwa wanawake, naye mtoto utakayemzaa amebarikiwa. 43 [q]Lakini ni kwa nini mimi nimepata upendeleo kiasi hiki, hata mama wa Bwana wangu afike kwangu? 44 Mara tu niliposikia sauti ya salamu yako, mtoto aliyeko tumboni mwangu aliruka kwa furaha. 45 [r]Amebarikiwa yeye aliyeamini kwamba lile Bwana alilomwambia litatimizwa."

*Wimbo Wa Maria Wa Sifa*

46 [s]Naye Maria akasema:

"Moyo wangu wamwadhimisha
Bwana,
47 [t]nayo roho yangu inamfurahia
Mungu Mwokozi wangu,
48 [u]kwa kuwa ameangalia kwa fadhili
unyonge wa mtumishi wake.

---

[a]**1:23** 2Fal 11:5
[b]**1:25** Mwa 30:23; Isa 4:1
[c]**1:26** Lk 1:62; Mt 2:23
[d]**1:27** Mt 1:16-20; Lk 2:4
[e]**1:28** Amu 5:24
[f]**1:29** Lk 1:12
[g]**1:30** Mt 14:27
[h]**1:31** Isa 7:14; Mt 1:21-25
[i]**1:32** Mk 5:7
[j]**1:33** Mt 28:18; 2Sam 7:16; Ebr 1:8
[k]**1:35** Mt 1:18; 4:3; Mk 1:24
[l]**1:36** Lk 1:24
[m]**1:37** Mt 19:26; Mwa 18:14; Zek 8:6; Mt 18:26; Mk 10:27; Rum 4:21
[n]**1:39** Lk 1:65; Yos 21:9, 10, 11
[o]**1:41** Lk 1:15; Mwa 25; 22
[p]**1:42** Amu 5:24
[q]**1:43** Yn 13:13
[r]**1:45** Lk 1:20; 11:28
[s]**1:46** Za 34:2-3
[t]**1:47** Za 18:46; 1Tim 4:10
[u]**1:48** Za 138:5; Lk 11:27

Hakika tangu sasa vizazi vyote
vitaniita aliyebarikiwa,
49 [a]kwa maana yeye Mwenye Nguvu
amenitendea mambo ya ajabu:
jina lake ni takatifu.
50 [b]Rehema zake huwaendea wale
wamchao,
kutoka kizazi hadi kizazi.
51 [c]Kwa kuwa ametenda mambo ya
ajabu kwa mkono wake;
amewatawanya wale wenye kiburi
ndani ya mioyo yao.
52 [d]Amewashusha watawala toka
kwenye viti vyao vya enzi,
lakini amewainua wanyenyekevu.
53 [e]Amewashibisha wenye njaa kwa
vitu vizuri,
bali matajiri amewafukuza mikono
mitupu.
54 [f]Amemsaidia mtumishi wake Israeli,
kwa kukumbuka ahadi yake ya
kumrehemu
55 [g]Abrahamu na uzao wake milele,
kama alivyowaahidi baba zetu."

56 Maria akakaa na Elizabeti karibu miezi
mitatu, kisha akarudi nyumbani kwake.

*Kuzaliwa Kwa Yohana Mbatizaji*

57 Ulipowadia wakati wa Elizabeti
kujifungua, alizaa mtoto mwanaume.
58 [h]Majirani zake na jamii zake wakasikia
jinsi Bwana alivyomfanyia rehema kuu, nao
wakafurahi pamoja naye.
59 [i]Siku ya nane wakaja kumtahiri mtoto,
wakataka yule mtoto aitwe Zekaria, ambalo
ndilo jina la baba yake. 60 [j]Lakini mama
yake akakataa na kusema, "Hapana! Jina
lake ataitwa Yohana."
61 Wakamwambia, "Hakuna mtu yeyote
katika jamaa yako mwenye jina kama hilo."
62 [k]Basi wakamfanyia Zekaria baba yake
ishara ili kujua kwamba yeye angependa
kumpa mtoto jina gani. 63 [l]Akaomba wampe
kibao cha kuandikia na kwa mshangao wa
kila mtu akaandika: "Jina lake ni Yohana."
64 [m]Papo hapo kinywa chake kikafunguliwa
na ulimi wake ukaachiwa, akawa anaongea
akimsifu Mungu. 65 Majirani wote wakajawa
na hofu ya Mungu, na katika nchi yote
ya vilima vya Uyahudi watu walikuwa
wakinena juu ya mambo haya yote. 66 [n]Kila
aliyesikia habari hizi alishangaa akauliza,
"Je, mtoto huyu atakuwa mtu wa namna
gani?" Maana mkono wa Bwana ulikuwa
pamoja naye.

*Unabii Wa Zekaria*

67 [o]Zekaria, baba yake, akajazwa na Roho
Mtakatifu, naye akatoa unabii, akisema:

68 [p]"Ahimidiwe Bwana, Mungu wa
Israeli,
kwa kuwa amewajilia watu wake
na kuwakomboa.
69 [q]Naye ametusimamishia pembe[r] ya
wokovu
katika nyumba ya Daudi mtumishi
wake,
70 [s]kama alivyonena kwa vinywa vya
manabii
wake watakatifu tangu zamani,
71 [t]kwamba atatuokoa kutoka kwa adui
zetu,
na kutoka mikononi mwao wote
watuchukiao:
72 [u]ili kuonyesha rehema kwa baba zetu
na kukumbuka Agano lake
takatifu,

---

[a] **1:49** Za 71:19; 111:9
[b] **1:50** Kut 20:6; Za 103:17
[c] **1:51** Za 98:1; Isa 40:10
[d] **1:52** Mt 23:12; 1Sam 2:6; Ay 5:11; Za 11:3, 6
[e] **1:53** Za 107:9; 1Sam 3:5
[f] **1:54** Za 98:3
[g] **1:55** Za 132:11; Gal 3:16
[h] **1:58** Lk 1:14
[i] **1:59** Law 12:3; Flp 3:5
[j] **1:60** Lk 1:13, 63; Mt 3:1
[k] **1:62** Lk 1:22
[l] **1:63** Lk 1:13, 60; Mt 3:1
[m] **1:64** Lk 1:20; Eze 24:27
[n] **1:66** Mwa 39:2; Mdo 11:21
[o] **1:67** Yoe 2:28
[p] **1:68** Mwa 24:27; 1Fal 8:15; Za 111:9; Lk 7:16
[q] **1:69** 2Sam 22:23; Za 132:17
[r] 69 Pembe hapa inamaanisha nguvu.
[s] **1:70** Yer 23:3; Za 132:17
[t] **1:71** Za 106:10
[u] **1:72** Mik 7:20; Za 106:45; Eze 16:60

73 [a]kiapo alichomwapia baba yetu
Abrahamu:
74 [b]kutuokoa kutoka mikononi mwa
adui zetu,
tupate kumtumikia yeye pasipo
hofu
75 [c]katika utakatifu na haki mbele zake,
siku zetu zote.

76 [d]"Nawe mtoto wangu, utaitwa nabii
wa Aliye Juu Sana;
kwa kuwa utamtangulia Bwana
na kuandaa njia kwa ajili yake,
77 [e]kuwajulisha watu wake juu ya
wokovu
utakaopatikana kwa kusamehewa
dhambi zao,
78 [f]kwa ajili ya wingi wa rehema za
Mungu wetu,
nuru itokayo juu itatuzukia
79 [g]ili kuwaangazia wale waishio gizani
na katika uvuli wa mauti,
kuiongoza miguu yetu katika njia ya
amani."

80 [h]Yule mtoto akakua na kuongezeka nguvu katika roho; akaishi nyikani hadi siku ile alipojionyesha hadharani kwa Waisraeli.

*Kuzaliwa Kwa Yesu*

**(Mathayo 1:18-25)**

2 [i]Siku zile Kaisari Augusto alitoa amri
kwamba watu wote waandikishwe
katika ulimwengu wa Kirumi. 2 [j](Orodha
hii ndiyo ya kwanza iliyofanyika wakati
Krenio alikuwa mtawala wa Shamu[k]). 3 Kila
mtu alikwenda kuandikishwa katika mji
wake alikozaliwa.
4 [l]Hivyo Yosefu akapanda kutoka mji wa
Nazareti ulioko Galilaya kwenda Uyahudi,
mpaka Bethlehemu, mji wa Daudi, kwa
sababu yeye alikuwa wa ukoo na wa
nyumba ya Daudi. 5 [m]Alikwenda huko
kujiandikisha pamoja na Maria, ambaye
alikuwa amemposa naye alikuwa mjamzito.
6 Wakiwa Bethlehemu, wakati wa Maria
wa kujifungua ukawa umetimia, 7 [n]naye
akamzaa mwanawe, kifungua mimba.
Akamfunika nguo za kitoto na kumlaza
katika hori ya kulia ng'ombe, kwa sababu
hapakuwa na nafasi katika nyumba ya
wageni.

*Wachungaji Na Malaika*

8 Katika eneo lile walikuwako wachungaji
waliokuwa wakikaa mashambani, wakilinda
makundi yao ya kondoo usiku. 9 [o]Ghafula
tazama, malaika wa Bwana akawatokea,
nao utukufu wa Bwana ukawang'aria
kotekote, wakaingiwa na hofu. 10 [p]Lakini
malaika akawaambia: "Msiogope. Kwa
maana tazama nawaletea habari njema
za furaha itakayokuwa kwa watu wote.
11 [q]Leo katika mji wa Daudi kwa ajili yenu
amezaliwa Mwokozi, ndiye Kristo[r] Bwana.
12 [s]Hii ndiyo itakayokuwa ishara kwenu:
Mtamkuta mtoto mchanga amefunikwa
nguo za kitoto na kulazwa katika hori ya
kulia ng'ombe."
13 [t]Ghafula pakawa na jeshi kubwa
la mbinguni pamoja na huyo malaika
wakimsifu Mungu wakisema,

14 [u]"Atukuzwe Mungu juu mbinguni,
na duniani iwe amani kwa watu
aliowaridhia."

15 Hao malaika walipokwisha kuondoka

[a]**1:73** Mwa 22:16-18
[b]**1:74** Ebr 9:14
[c]**1:75** Efe 4:24
[d]**1:76** Mt 11:9; Mk 5:7; Mal 3:1; Mt 3:3
[e]**1:77** Yer 31:34; Mt 1:21
[f]**1:78** Mal 4:2
[g]**1:79** Za 107:14; Mdo 26:18
[h]**1:80** Lk 2:40, 52
[i]**2:1** Lk 3:1; Mt 22:17; 24:14
[j]**2:2** Mdo 21:3; Mt 4:24; Mdo 15:23, 41
[k]2 Shamu inamaanisha Syria.
[l]**2:4** Yn 7:42
[m]**2:5** Lk 1:27; Mt 1:16
[n]**2:7** Mt 1:25
[o]**2:9** Lk 1:11; Mdo 5:19
[p]**2:10** Mt 14:27
[q]**2:11** Yn 3:17; Rum 11:14; Mdo 3:20; 9:22
[r]11 *Kristo* maana yake ni *Masiya,* yaani *Aliyetiwa mafuta.*
[s]**2:12** 1Sam 10:7; Za 86:17
[t]**2:13** Dan 7:10; Mwa 28:12; 32:12; Za 103:20, 21; 148:2; Ebr 1:14; Ufu 5:11
[u]**2:14** Isa 9:6; Rum 5:1

na kwenda zao mbinguni, wale wachungaji
wakasemezana wao kwa wao, “Twendeni
Bethlehemu tukaone mambo haya ya ajabu
yaliyotukia, ambayo Bwana ametuambia
habari zake.”
16 [a]Hivyo wakaenda haraka Bethlehemu,
wakawakuta Maria na Yosefu na yule
mtoto mchanga akiwa amelala katika hori
la kulia ng’ombe. 17 [b]Walipomwona yule
mtoto, wakawaeleza yale waliyokuwa
wameambiwa kuhusu huyo mtoto. 18 Nao
wote waliosikia habari hizi wakastaajabia
yale waliyoambiwa na wale wachungaji wa
kondoo. 19 [c]Lakini Maria akayaweka mambo
haya yote moyoni mwake na kuyatafakari.
20 [d]Wale wachungaji wakarudi, huku
wakimtukuza Mungu na kumsifu kwa ajili
ya mambo yote waliyokuwa wameambiwa
na kuyaona.
21 [e]Hata zilipotimia siku nane, ulikuwa
ndio wakati wa kumtahiri mtoto, akaitwa
Yesu, jina alilokuwa amepewa na malaika
kabla hajatungwa mimba.

### *Yesu Apelekwa Hekaluni*

22 [f]Ulipotimia wakati wa utakaso wake
Maria kwa mujibu wa Sheria ya Mose,
basi Yosefu na Maria walimpeleka mtoto
Yerusalemu, ili kumweka wakfu kwa
Bwana 23 [g](kama ilivyoandikwa katika
Sheria ya Bwana, kwamba, “Kila mtoto wa
kiume kifungua mimba atawekwa wakfu
kwa Bwana”), 24 [h]na pia kutoa dhabihu
kulingana na yale yaliyonenwa katika
Sheria ya Bwana: “Hua wawili au makinda
mawili ya njiwa.”
25 [i]Basi alikuwako huko Yerusalemu mtu
mmoja jina lake Simeoni, ambaye alikuwa
mwenye haki na mcha Mungu, akitarajia
faraja ya Israeli, na Roho Mtakatifu
alikuwa juu yake. 26 [j]Roho Mtakatifu
alikuwa amemfunulia kuwa hatakufa kabla
hajamwona Kristo wa Bwana. 27 [k]Simeoni,
akiwa ameongozwa na Roho Mtakatifu,
alikwenda Hekaluni. Wazazi walipomleta
mtoto Yesu ili kumfanyia kama ilivyokuwa
desturi ya Sheria, 28 ndipo Simeoni
akampokea mtoto mikononi mwake na
kumsifu Mungu, akisema:

29 [l]“Bwana Mwenyezi, kama
ulivyoahidi,
sasa wamruhusu mtumishi wako
aende zake kwa amani.
30 [m]Kwa maana macho yangu yameuona
wokovu wako,
31 ulioweka tayari machoni pa watu
wote,
32 [n]nuru kwa ajili ya ufunuo kwa watu
wa Mataifa
na kwa ajili ya utukufu kwa watu
wako Israeli.”

33 Naye Yosefu na mama yake mtoto
wakastaajabu kwa yale yaliyokuwa
yamesemwa kumhusu huyo mtoto. 34 [o]Kisha
Simeoni akawabariki, akamwambia Maria
mama yake, “Mtoto huyu amewekwa
kwa makusudi ya kuanguka na kuinuka
kwa wengi katika Israeli. Atakuwa ishara
ambayo watu watanena dhidi yake, 35 [p]ili
mawazo ya mioyo mingi yadhihirike. Nao
upanga utauchoma moyo wako.”
36 [q]Tena alikuwako Hekaluni nabii mmoja
mwanamke, jina lake Ana binti Fanueli,
wa kabila la Asheri. Alikuwa mzee sana;
naye alikuwa ameolewa na kuishi na mume
kwa miaka saba tu, kisha mumewe akafa.
37 [r]Hivyo alikuwa mjane na umri wake
ulikuwa miaka themanini na minne. Yeye
hakuondoka humo Hekaluni usiku wala
mchana, bali alikuwa akimwabudu Mungu,

[a]**2:16** Lk 2:7
[b]**2:17** Lk 2:10-12
[c]**2:19** Lk 2:51
[d]**2:20** Mt 9:8
[e]**2:21** Lk 1:31, 59
[f]**2:22** Law 12:2-8
[g]**2:23** Kut 2:12-15; Hes 3:13
[h]**2:24** Law 12:8
[i]**2:25** Lk 16:6; 23:51; Isa 52:9
[j]**2:26** Za 89:48; Ebr 11:5
[k]**2:27** Mwa 46:30; Flp 1:23; Lk 2:22
[l]**2:29** Mdo 2:24
[m]**2:30** Isa 40:5; Lk 3:6; Isa 52:10
[n]**2:32** Isa 49:6; Mdo 26:23
[o]**2:34** Mt 12:46; Isa 8:14; Gal 5:11
[p]**2:35** Za 42:10; Yn 19:25
[q]**2:36** Mdo 21:9
[r]**2:37** 1Tim 5:9; Mdo 14:23

akifunga na kuomba. 38 [a]Wakati huo huo,
Ana alikuja akaanza kusifu, akimshukuru
Mungu na kusema habari za huyo mtoto
kwa watu wote waliokuwa wakitarajia
ukombozi wa Yerusalemu.
39 [b]Yosefu na Maria walipokuwa
wamekamilisha mambo yote yaliyotakiwa
na Sheria ya Bwana, walirudi mjini kwao
Nazareti huko Galilaya. 40 [c]Naye yule mtoto
akakua na kuongezeka nguvu, akiwa amejaa
hekima, na neema ya Mungu ilikuwa juu
yake.

*Kijana Yesu Hekaluni*

41 [d]Kila mwaka Yosefu na Maria mama
yake Yesu walikuwa na desturi ya kwenda
Yerusalemu kwa ajili ya Sikukuu ya Pasaka.
42 Yesu alipokuwa na umri wa miaka kumi na
miwili, walipanda kwenda kwenye Sikukuu
hiyo kama ilivyokuwa desturi. 43 [e]Baada
ya Sikukuu kumalizika, wakati Yosefu na
Maria mama yake walipokuwa wakirudi
nyumbani, Yesu alibaki Yerusalemu lakini
hawakutambua. 44 Wao wakidhani kuwa
yuko miongoni mwa wasafiri, walienda
mwendo wa kutwa nzima. Ndipo wakaanza
kumtafuta miongoni mwa jamaa zao
na marafiki. 45 Walipomkosa walirudi
Yerusalemu ili kumtafuta. 46 Baada ya siku
tatu wakamkuta ndani ya Hekalu, akiwa
ameketi katikati ya walimu wa sheria,
akiwasikiliza na kuwauliza maswali.
47 [f]Wote waliomsikia walistaajabishwa
na uwezo wake mkubwa wa kuelewa, na
majibu aliyoyatoa. 48 [g]Yosefu na Maria
mama yake walipomwona walishangaa.
Mama yake akamuuliza, "Mwanangu,
mbona umetufanyia hivi? Tazama, mimi
na baba yako tumekuwa tukikutafuta kwa
wasiwasi mkubwa kila mahali."
49 [h]Yesu akawaambia, "Kwa nini
kunitafuta? Hamkujua kwamba imenipasa
kuwa katika nyumba ya Baba yangu?"
50 [i]Lakini wao hawakuelewa maana ya
lile alilowaambia.
51 [j]Ndipo akashuka pamoja nao hadi
Nazareti, naye alikuwa mtiifu kwao. Lakini
mama yake akayaweka moyoni mwake
mambo haya yote. 52 [k]Naye Yesu akakua
katika hekima na kimo, akimpendeza
Mungu na wanadamu.

*Yohana Mbatizaji Aanza Kuhubiri*

**(Mathayo 3:1-12; Marko 1:1-8;
Yohana 1:19-28)**

3 [l]Katika mwaka wa kumi na tano wa
utawala wa Kaisari Tiberio, Pontio
Pilato akiwa mtawala wa Uyahudi, Herode
akiwa mfalme wa Galilaya, Filipo ndugu
yake akiwa mfalme wa Iturea na nchi ya
Trakoniti, na Lisania akiwa mfalme wa
Abilene, 2 [m]nao Anasi na Kayafa wakiwa
makuhani wakuu, neno la Mungu likamjia
Yohana, mwana wa Zekaria huko jangwani.
3 [n]Akaenda katika nchi yote kandokando
ya Mto Yordani, akihubiri ubatizo wa toba
kwa ajili ya msamaha wa dhambi. 4 [o]Kama
ilivyoandikwa katika kitabu cha nabii Isaya:

"Sauti ya mtu aliaye nyikani,
'Itengenezeni njia ya Bwana,
yanyoosheni mapito yake.
5 Kila bonde litajazwa,
kila mlima na kilima vitashushwa.
Njia zilizopinda zitanyooshwa,
na zilizoparuza zitasawazishwa.
6 [p]Nao watu wote watauona
wokovu wa Mungu.' "

7 [q]Yohana akauambia ule umati wa watu
uliokuwa unakuja ili kubatizwa naye, "Ninyi
watoto wa nyoka! Ni nani aliyewaonya

[a]**2:38** Isa 52:9; Lk 24:21
[b]**2:39** Mt 2:23
[c]**2:40** Lk 2:52; 1:80
[d]**2:41** Kut 23:15; Lk 22:8
[e]**2:43** Kut 12:18
[f]**2:47** Mt 7:28
[g]**2:48** Mt 12:46; Lk 3:23; 4:22
[h]**2:49** Yn 2:16
[i]**2:50** Mk 9:32
[j]**2:51** Lk 2:19
[k]**2:52** Mit 3; 4; Lk 1:80
[l]**3:1** Mt 27:2
[m]**3:2** Yn 18:13; Mdo 4:6; Mt 3:1
[n]**3:3** Mk 3:16; Mal 1:4
[o]**3:4** Isa 40:3-5; Mt 3:3; Mk 1:3; Yn 1:23
[p]**3:6** Za 98:2; Lk 2:30
[q]**3:7** Mt 12:34; 23:33; Rum 1:18

kuikimbia ghadhabu inayokuja? 8 [a]Basi
zaeni matunda yastahiliyo toba. Wala
msianze kusema mioyoni mwenu kuwa,
‘Sisi tunaye Abrahamu, baba yetu.’ Kwa
maana nawaambia kuwa Mungu anaweza
kumwinulia Abrahamu watoto kutoka mawe
haya. 9 [b]Hata sasa shoka limeshawekwa
tayari kwenye shina la kila mti. Basi kila
mti usiozaa matunda mazuri hukatwa na
kutupwa motoni.”

10 [c]Ule umati wa watu ukamuuliza,
“Inatupasa tufanyeje basi?”

11 [d]Yohana akawaambia, “Aliye na kanzu
mbili amgawie asiye nayo, naye aliye na
chakula na afanye vivyo hivyo.”

12 [e]Watoza ushuru nao wakaja ili
wabatizwe, wakamuuliza, “Bwana na sisi
inatupasa tufanyeje?”

13 [f]Akawaambia, “Msichukue zaidi ya
kiwango mlichopangiwa.”

14 [g]Askari nao wakamuuliza, “Je, nasi
inatupasa tufanye nini?”

Akawaambia, “Msimdhulumu mtu wala
msimshtaki mtu kwa uongo, bali mridhike
na mishahara yenu.”

15 [h]Watu walikuwa na matazamio
makubwa. Wakawa wanajiuliza mioyoni
mwao iwapo Yohana angeweza kuwa ndiye
Kristo.[i] 16 [j]Yohana akawajibu akawaambia,
“Mimi nawabatiza kwa maji.[k] Lakini
atakuja aliye na nguvu kuniliko mimi,
ambaye sistahili hata kufungua kamba za
viatu vyake. Yeye atawabatiza kwa Roho
Mtakatifu na kwa moto. 17 [l]Pepeto lake liko
mkononi, tayari kusafisha sakafu yake ya
kupuria na kuikusanya ngano ghalani,
lakini makapi atayateketeza kwa moto
usiozimika.” 18 Basi, kwa maonyo mengine
mengi Yohana aliwasihi na kuwahubiria
watu Habari Njema.

19 [m]Lakini Yohana alipomkemea Mfalme
Herode kuhusu uhusiano wake na Herodia,
mke wa ndugu yake, na maovu mengine
aliyokuwa amefanya, 20 [n]Herode aliongezea
jambo hili kwa hayo mengine yote:
alimfunga Yohana gerezani.

### *Kubatizwa Kwa Bwana Yesu*

**(Mathayo 3:13-17; Marko 1:9-11)**

21 [o]Baada ya watu wote kubatizwa,
Yesu naye akabatizwa. Naye alipokuwa
akiomba, mbingu zilifunguka. 22 [p]Roho
Mtakatifu akashuka juu yake kwa umbo
kama la hua, nayo sauti kutoka mbinguni
ikasema: “Wewe ni Mwanangu mpendwa;
nami nimependezwa nawe sana.”

### *Ukoo Wa Bwana Yesu*

**(Mathayo 1:1-17)**

23 [q]Yesu alikuwa na umri wa miaka
thelathini alipoanza huduma yake. Alikuwa
akidhaniwa kuwa mwana wa Yosefu,

Yosefu alikuwa mwana wa Eli,
24 Eli alikuwa mwana wa Mathati,
Mathati alikuwa mwana wa Lawi,
Lawi alikuwa mwana wa Melki,
Melki alikuwa mwana wa Yanai,
Yanai alikuwa mwana wa Yosefu,
25 Yosefu alikuwa mwana wa Matathia,
Matathia alikuwa mwana wa Amosi,
Amosi alikuwa mwana wa Nahumu,
Nahumu alikuwa mwana wa Esli,
Esli alikuwa mwana wa Nagai,
26 Nagai alikuwa mwana wa Maathi,
Maathi alikuwa mwana wa Matathia,
Matathia alikuwa mwana wa
Semeini,
Semeini alikuwa mwana wa Yoseki,
Yoseki alikuwa mwana wa Yoda,
27 [r]Yoda alikuwa mwana wa Yoanani,
Yoanani alikuwa mwana wa Resa,

[a]**3:8** Isa 51:7; Gal 3:7
[b]**3:9** Mt 3:10
[c]**3:10** Mdo 2:37; 16:30
[d]**3:11** Isa 58:7; Eze 18:7
[e]**3:12** Lk 7:29
[f]**3:13** Lk 19:8
[g]**3:14** Law 19:11
[h]**3:15** Mt 3:1; Yn 1:19-20; Mdo 13:25
[i]15 *Kristo* maana yake ni *Masiya*, yaani *Aliyetiwa mafuta.*
[j]**3:16** Mk 1:4; Yn 1:26, 33; Mdo 11:16
[k]16 Tafsiri nyingine zinasema ndani ya maji.
[l]**3:17** Isa 30:24; Mt 13:30; 25:41
[m]**3:19** Mt 14:1
[n]**3:20** Mt 14:3-4
[o]**3:21** Mt 14:23; Mk 1:35
[p]**3:22** Isa 42:1; Yn 1:32-33; Mt 3:17
[q]**3:23** Mt 4:17; Lk 1:27
[r]**3:27** Mt 1:12; 1Nya 3:17

Resa alikuwa mwana wa Zerubabeli,
Zerubabeli alikuwa mwana wa Shealtieli,
Shealtieli alikuwa mwana wa Neri,
28 Neri alikuwa mwana wa Melki,
Melki alikuwa mwana wa Adi,
Adi alikuwa mwana wa Kosamu,
Kosamu alikuwa mwana wa Elmadamu,
Elmadamu alikuwa mwana wa Eri,
29 Eri alikuwa mwana wa Yoshua,
Yoshua alikuwa mwana wa Eliezeri,
Eliezeri alikuwa mwana wa Yorimu,
Yorimu alikuwa mwana wa Mathati,
Mathati alikuwa mwana wa Lawi,
30 Lawi alikuwa mwana wa Simeoni,
Simeoni alikuwa mwana wa Yuda,
Yuda alikuwa mwana wa Yosefu,
Yosefu alikuwa mwana wa Yonamu,
Yonamu alikuwa mwana wa Eliakimu,
Eliakimu alikuwa mwana wa Melea,
31 [a]Melea alikuwa mwana wa Mena,
Mena alikuwa mwana wa Matatha,
Matatha alikuwa mwana wa Nathani,
Nathani alikuwa mwana wa Daudi,
32 [b]Daudi alikuwa mwana wa Yese,
Yese alikuwa mwana wa Obedi,
Obedi alikuwa mwana wa Boazi,
Boazi alikuwa mwana wa Salmoni,
Salmoni alikuwa mwana wa Nashoni,
33 [c]Nashoni alikuwa mwana wa Aminadabu,
Aminadabu alikuwa mwana wa Aramu,
Aramu alikuwa mwana wa Hesroni,
Hesroni alikuwa mwana wa Peresi,
Peresi alikuwa mwana wa Yuda,
34 [d]Yuda alikuwa mwana wa Yakobo,
Yakobo alikuwa mwana wa Isaki,
Isaki alikuwa mwana wa Abrahamu,
Abrahamu alikuwa mwana wa Tera,
Tera alikuwa mwana wa Nahori,
35 Nahori alikuwa mwana wa Serugi,

[a]**3:31** 2Sam 5:14; 1Nya 3:5
[b]**3:32** Rut 4:22; 1Nya 2:10
[c]**3:33** Rut 4:18-22; 1Nya 2:10
[d]**3:34** Mwa 11:24-26

Serugi alikuwa mwana wa Reu,
Reu alikuwa mwana wa Pelegi,
Pelegi alikuwa mwana wa Eberi,
Eberi alikuwa mwana wa Sala,
36 [e]Sala alikuwa mwana wa Kenani,
Kenani alikuwa mwana wa Arfaksadi,
Arfaksadi alikuwa mwana wa Shemu,
Shemu alikuwa mwana wa Noa,
Noa alikuwa mwana wa Lameki,
37 [f]Lameki alikuwa mwana wa Methusela,
Methusela alikuwa mwana wa Enoki,
Enoki alikuwa mwana wa Yaredi,
Yaredi alikuwa mwana wa Mahalaleli,
Mahalaleli alikuwa mwana wa Kenani,
38 [g]Kenani alikuwa mwana wa Enoshi,
Enoshi alikuwa mwana wa Sethi,
Sethi alikuwa mwana wa Adamu,
Adamu alikuwa mwana wa Mungu.

### *Yesu Ajaribiwa Na Shetani*

**(Mathayo 4:1-11; Marko 1:12-13)**

4 [h]Yesu, akiwa amejaa Roho Mtakatifu,
akarudi kutoka Yordani. Akaongozwa
na Roho Mtakatifu hadi nyikani, 2 [i]mahali
ambako kwa siku arobaini alikuwa
akijaribiwa na ibilisi. Kwa siku zote hizo
hakula chochote, hivyo baada ya muda huo
akaona njaa.
3 [j]Ibilisi akamwambia, “Ikiwa wewe ni
Mwana wa Mungu, amuru jiwe hili liwe
mkate.”
4 [k]Yesu akajibu akamwambia,
“Imeandikwa: ‘Mtu haishi kwa mkate tu.’ ”
5 [l]Ibilisi akampeleka hadi juu ya mlima
mrefu akamwonyesha milki zote za dunia
kwa mara moja. 6 [m]Akamwambia, “Nitakupa

[e]**3:36** Mwa 5:28-32; 11:12
[f]**3:37** Mwa 5:12-25
[g]**3:38** Mwa 5:19
[h]**4:1** Lk 1:15-45; 3:3-21; Eze 37:1; Lk 2:27
[i]**4:2** Kut 34:28; 1Fal 19:8
[j]**4:3** Mt 4:3
[k]**4:4** Kum 8:3
[l]**4:5** Mt 24:14
[m]**4:6** Yn 14:30

mamlaka juu ya milki hizi na fahari zake
zote, kwa maana zimekabidhiwa mkononi
mwangu nami ninaweza kumpa yeyote
ninayetaka. 7 Hivyo ikiwa utanisujudia na
kuniabudu, vyote vitakuwa vyako.”
8 [a]Yesu akamjibu, “Imeandikwa:
‘Mwabudu Bwana Mungu wako na
umtumikie yeye peke yake.’ ”
9 [b]Kisha ibilisi akampeleka mpaka
Yerusalemu, akamweka juu ya mnara
mrefu wa Hekalu, akamwambia, “Kama
wewe ndiwe Mwana wa Mungu, jitupe chini
kutoka hapa, 10 [c]kwa maana imeandikwa:

“ ‘Atakuagizia malaika zake
ili wakulinde;
11 [d]nao watakuchukua mikononi mwao,
usije ukajikwaa mguu wako katika
jiwe.’ ”

12 [e]Yesu akamjibu, “Imesemwa,
‘Usimjaribu Bwana Mungu wako.’ ”
13 [f]Ibilisi alipomaliza kila jaribu,
akamwacha Yesu mpaka wakati mwingine
ufaao.

*Mwanzo Wa Huduma Ya Galilaya*

**(Mathayo 4:12-17; Marko 1:14-15)**

14 [g]Kisha Yesu akarudi mpaka Galilaya,
akiwa amejaa nguvu za Roho Mtakatifu,
nazo habari zake zikaenea katika sehemu
zote za nchi za kandokando. 15 [h]Akaanza
kufundisha kwenye masinagogi yao, na kila
mmoja akamsifu.

*Yesu Akataliwa Nazareti*

**(Mathayo 13:53-58; Marko 6:1-6)**

16 [i]Yesu akaenda Nazareti, alipolelewa, na
siku ya Sabato alikwenda katika sinagogi
kama ilivyokuwa desturi yake. Akasimama
ili asome, 17 [j]naye akapewa kitabu cha
nabii Isaya, akakifungua na kukuta mahali
palipoandikwa:

18 [k]“Roho wa Bwana yu juu yangu,
kwa sababu amenitia mafuta
kuwahubiria maskini habari
njema.
Amenituma kuwatangazia wafungwa
kufunguliwa kwao,
na vipofu kupata kuona tena,
kuwaweka huru wanaoonewa,
19 na kutangaza mwaka wa Bwana
uliokubalika.”

20 [l]Kisha akakifunga kitabu, akamrudishia
mtumishi na akaketi. Watu wote
waliokuwamo katika sinagogi wakamkazia
macho. 21 [m]Ndipo akaanza kwa kuwaambia,
“Leo Andiko hili limetimia mkiwa
mnasikia.”
22 [n]Wote waliokuwako wakamsifu na
kuyastaajabia maneno yake yaliyojaa
neema, wakaulizana, “Je, huyu si mwana
wa Yosefu?”
23 [o]Yesu akawaambia, “Bila shaka
mtatumia mithali hii: ‘Tabibu, jiponye
mwenyewe! Mambo yale tuliyosikia
kwamba uliyafanya huko Kapernaumu,
yafanye na hapa kwenye mji wako.’ ”
24 [p]Yesu akasema, “Amin, nawaambia,
hakuna nabii anayekubalika katika mji wake
mwenyewe. 25 [q]Lakini ukweli ni kwamba
palikuwa na wajane wengi katika Israeli
wakati wa Eliya, mbingu zilipofungwa kwa
miaka mitatu na miezi sita pakawa na njaa
kuu katika nchi nzima. 26 [r]Hata hivyo Eliya
hakutumwa hata kwa mmoja wao, bali kwa
mjane mmoja wa Sarepta katika nchi ya
Sidoni. 27 [s]Pia palikuwa na wengi wenye
ukoma katika Israeli katika siku za nabii
Elisha, lakini hakuna hata mmoja wao

[a]**4:8** Kum 6:3
[b]**4:9** Mt 4:5
[c]**4:10** Za 91:11, 12
[d]**4:11** Za 91:12
[e]**4:12** Kum 6:12
[f]**4:13** Ebr 4:15; Yn 14:30
[g]**4:14** Mt 4:12; 9:26
[h]**4:15** Mt 4:23
[i]**4:16** Mt 2:23; 13:54
[j]**4:17** Isa 61:1, 2; 58:6
[k]**4:18** Yn 3:34
[l]**4:20** Mt 26:55
[m]**4:21** Mt 1:22
[n]**4:22** Yn 6:42; 7:15
[o]**4:23** Mt 2:23; Mk 1:21-28; 2:1-12
[p]**4:24** Mt 13:57; Yn 4:44
[q]**4:25** 1Fal 18:1; Ufu 11:6
[r]**4:26** 1Fal 17:8-16; Mt 11:21
[s]**4:27** 2Fal 5:1-14

aliyetakaswa, isipokuwa Naamani mtu wa
Shamu."[a]
28 Watu wote katika sinagogi waliposikia
maneno haya, wakakasirika sana.
29 [b]Wakasimama, wakamtoa nje ya mji,
wakamchukua hadi kwenye kilele cha
mlima mahali ambapo mji huo ulikuwa
umejengwa, ili wamtupe chini kutoka
kwenye mteremko mkali. 30 [c]Lakini yeye
akapita papo hapo katikati ya huo umati
wa watu akaenda zake.

*Yesu Atoa Pepo Mchafu*

**(Marko 1:21-28)**

31 [d]Kisha Yesu akashuka kwenda
Kapernaumu, mji wa Galilaya, na katika
siku ya Sabato akawa anafundisha.
32 [e]Wakashangazwa sana na mafundisho
yake, maana maneno yake yalikuwa na
mamlaka.
33 [f]Ndani ya sinagogi palikuwa na mtu
aliyekuwa amepagawa na pepo mchafu.
Naye akapiga kelele kwa nguvu akisema,
34 [g]"Tuache! Tuna nini nawe, Yesu wa
Nazareti? Je, umekuja kutuangamiza?
Ninakujua wewe ni nani. Wewe ndiwe Aliye
Mtakatifu wa Mungu!"
35 [h]Basi Yesu akamkemea yule pepo
mchafu, akisema, "Nyamaza kimya! Nawe
umtoke!" Yule pepo mchafu akamwangusha
yule mtu chini mbele yao wote, akatoka
pasipo kumdhuru. 36 [i]Watu wote
wakashangaa, wakaambiana, "Mafundisho
haya ni ya namna gani? Anawaamuru pepo
wachafu kwa mamlaka na nguvu, nao
wanatoka!" 37 [j]Habari zake zikaanza kuenea
kila mahali katika sehemu ile.

*Yesu Awaponya Wengi*

**(Mathayo 8:14-17; Marko 1:29-34)**

38 [k]Yesu akatoka katika sinagogi, akaenda
nyumbani kwa Simoni. Basi huko alimkuta
mama mkwe wa Simoni akiwa ameshikwa
na homa kali, nao wakamwomba Yesu
amsaidie. 39 [l]Hivyo Yesu akamwinamia
na kukemea ile homa, nayo ikamwacha.
Akaamka saa ile ile, naye akaanza
kuwahudumia.
40 [m]Jua lilipokuwa linatua, watu
wakamletea Yesu watu wote waliokuwa
na maradhi mbalimbali, naye akaweka
mikono yake juu ya kila mgonjwa,
naye akawaponya. 41 [n]Pepo wachafu pia
wakawatoka watu wengi, nao walipokuwa
wakitoka wakapiga kelele, wakisema:
"Wewe ni Mwana wa Mungu!" Lakini Yesu
akawakemea na kuwazuia wasiseme, kwa
maana walimjua kuwa yeye ndiye Kristo.[o]
42 [p]Kesho yake, kulipopambazuka, Yesu
alikwenda mahali pa faragha. Watu
wengi wakawa wanamtafuta kila mahali,
nao walipomwona wakajaribu kumzuia
asiondoke. 43 [q]Lakini yeye akawaambia,
"Imenipasa kuhubiri habari njema za Ufalme
wa Mungu katika miji mingine pia, kwa
maana kwa kusudi hili nilitumwa." 44 [r]Naye
aliendelea kuhubiri katika masinagogi ya
Uyahudi.

*Kuitwa Kwa Wanafunzi Wa Kwanza*

**(Mathayo 4:18-22; Marko 1:16-20)**

5 [s]Siku moja Yesu alipokuwa amesimama
karibu na Ziwa la Genesareti,[t] watu
wengi wakiwa wanasongana kumzunguka
ili wapate kusikia neno la Mungu, 2 akaona
mashua mbili ukingoni mwa ziwa, zikiwa
zimeachwa hapo na wavuvi waliokuwa

[a]27 Shamu hapa inamaanisha Syria.
[b]**4:29** Hes 15:35; Ebr 13:12
[c]**4:30** Yn 8:59; 10:39
[d]**4:31** Mt 4:13
[e]**4:32** Mt 7:28-29
[f]**4:33** Mk 1:23
[g]**4:34** Mt 8:28-29; Mk 1:24; Yak 2:19
[h]**4:35** Mt 8:26; Lk 8:24
[i]**4:36** Mt 7:28-29; 10:1
[j]**4:37** Mt 9:26
[k]**4:38** Mt 8:14; Mk 1:29
[l]**4:39** Lk 4:35, 41
[m]**4:40** Mk 5:23; Mt 4:23
[n]**4:41** Mt 4:3; 8:4
[o]41 *Kristo* maana yake ni *Masiya*, yaani *Aliyetiwa mafuta.*
[p]**4:42** Mk 1:35
[q]**4:43** Mt 3:2
[r]**4:44** Mt 4:23
[s]**5:1** Mk 4:14; Ebr 4:12
[t]1 Yaani Bahari ya Galilaya.

wanaosha nyavu zao. 3 [a]Akaingia katika
mojawapo ya hizo mashua ambayo ilikuwa
ya Simoni, akamwomba aisogeze ndani ya
maji kidogo kutoka ufuoni. Kisha akaketi
na kufundisha watu akiwa mle ndani ya
mashua.
4 [b]Alipomaliza kunena, akamwambia
Simoni, "Sasa peleka mashua hadi kilindini
kisha mshushe nyavu zenu mkavue samaki."
5 [c]Simoni akamjibu, "Bwana, tumefanya
kazi ya kuchosha usiku kucha na
hatukuvua chochote. Lakini, kwa neno lako
nitazishusha nyavu."
6 [d]Nao walipozishusha nyavu zao,
wakavua samaki wengi sana, nyavu zao
zikajaa zikaanza kukatika. 7 Wakawaashiria
wavuvi wenzao kwenye ile mashua nyingine
ili waje kuwasaidia. Wakaja, wakajaza
mashua zote mbili samaki hata zikaanza
kuzama.
8 [e]Simoni Petro alipoona haya
yaliyotukia, alianguka miguuni mwa Yesu
na kumwambia, "Bwana, ondoka kwangu.
Mimi ni mtu mwenye dhambi!" 9 Kwa
kuwa yeye na wavuvi wenzake walikuwa
wameshangazwa sana na wingi wa samaki
waliokuwa wamepata. 10 [f]Vivyo hivyo
wenzake Simoni, yaani Yakobo na Yohana,
wana wa Zebedayo, walishangazwa pia.
Ndipo Yesu akamwambia Simoni,
"Usiogope, tangu sasa utakuwa mvuvi wa
watu." 11 [g]Hivyo wakasogeza mashua zao
mpaka ufuoni mwa bahari, wakaacha kila
kitu na kumfuata.

*Yesu Amtakasa Mtu Mwenye Ukoma*

**(Mathayo 8:1-4; Marko 1:40-45)**

12 [h]Ikawa siku moja Yesu alipokuwa katika
mji fulani, mtu mmoja mwenye ukoma
mwili mzima akamjia. Alipomwona Yesu,
alianguka chini mpaka uso wake ukagusa
ardhi, akamsihi akisema, "Bwana, ukitaka,
waweza kunitakasa."
13 Yesu akanyoosha mkono wake,
akamgusa yule mtu, akamwambia,
"Nataka. Takasika!" Na mara ukoma wake
ukatakasika.
14 [i]Yesu akamwagiza akisema,
"Usimwambie mtu yeyote, bali nenda
ukajionyeshe kwa kuhani na ukatoe sadaka
alizoagiza Mose kwa utakaso wako, ili kuwa
ushuhuda kwao."
15 [j]Lakini habari zake Yesu zikazidi sana
kuenea kotekote kuliko wakati mwingine
wowote. Makutano makubwa ya watu
yalikuwa yakikusanyika ili kumsikiliza na
kuponywa magonjwa yao. 16 [k]Lakini mara
kwa mara Yesu alijitenga nao ili kwenda
mahali pa faragha kuomba.

*Yesu Amponya Mtu Mwenye Kupooza*

**(Mathayo 9:1-8; Marko 2:1-12)**

17 [l]Siku moja Yesu alipokuwa akifundisha,
Mafarisayo na walimu wa sheria, waliokuwa
wametoka kila kijiji cha Galilaya na
kutoka Uyahudi na Yerusalemu, walikuwa
wameketi huko. Nao uweza wa Bwana
ulikuwa juu yake kuponya wagonjwa.
18 [m]Wakaja watu wamembeba mgonjwa
aliyepooza kwenye mkeka. Wakajaribu
kumwingiza ndani ili wamweke mbele ya
Yesu. 19 Walipokuwa hawawezi kufanya
hivyo kwa sababu ya umati wa watu,
wakapanda juu ya paa, wakaondoa baadhi
ya matofali, wakamteremsha yule mgonjwa
kwa mkeka wake hadi katikati ya ule umati
pale mbele ya Yesu.
20 [n]Yesu alipoiona imani yao, akamwambia
yule mgonjwa, "Rafiki, dhambi zako
zimesamehewa."
21 [o]Mafarisayo na wale walimu wa sheria
wakaanza kuuliza, "Ni nani mtu huyu
anayesema maneno ya kukufuru? Ni nani

[a]**5:3** Mt 13:2
[b]**5:4** Yn 21:6
[c]**5:5** Lk 9:33, 49; 17:13; Yn 21:3
[d]**5:6** Yn 21:11
[e]**5:8** Mwa 18:27; Ay 42:6
[f]**5:10** Mt 14:27
[g]**5:11** Mt 4:11
[h]**5:12** Mt 8:12
[i]**5:14** Mt 8:4
[j]**5:15** Mt 9:26
[k]**5:16** Mt 14:23
[l]**5:17** Mt 15:1; Lk 2:46; Mk 5:30; Lk 6:19
[m]**5:18** Mt 9:2; Mk 2:8
[n]**5:20** Lk 7:48-49
[o]**5:21** Isa 43:25; Lk 7:49; Yn 5:12

awezaye kusamehe dhambi isipokuwa
Mungu peke yake?”
22 Yesu akijua mawazo yao akawauliza,
“Kwa nini mnawaza hivyo mioyoni mwenu?
23 Je, ni lipi lililo rahisi zaidi, kumwambia,
‘Umesamehewa dhambi zako,’ au kusema,
‘Inuka, uende’? 24 [a]Lakini ili mpate kujua
kwamba Mwana wa Adamu anayo mamlaka
duniani kusamehe dhambi…” Akamwambia
yule aliyepooza, “Nakuambia, inuka,
chukua mkeka wako, uende nyumbani
kwako.” 25 Mara yule mtu aliyekuwa
amepooza akasimama mbele yao wote,
akachukua mkeka wake, akaenda zake
nyumbani, huku akimtukuza Mungu. 26 [b]Kila
mmoja akashangaa na kumtukuza Mungu.
Wakajawa na hofu ya Mungu, wakasema,
“Leo tumeona mambo ya ajabu.”

*Yesu Amwita Lawi*

**(Mathayo 9:9-13; Marko 2:13-17)**

27 [c]Baada ya haya, Yesu alitoka na
kumwona mtoza ushuru mmoja jina lake
Lawi akiwa amekaa forodhani, mahali pake
pa kutoza ushuru. Akamwambia, “Nifuate.”
28 [d]Naye Lawi akaacha kila kitu, akaondoka,
akamfuata.
29 [e]Kisha Lawi akamfanyia Yesu karamu
kubwa nyumbani kwake, nao umati
mkubwa wa watoza ushuru na watu wengine
walikuwa wakila pamoja nao. 30 [f]Lakini
Mafarisayo na walimu wa sheria waliokuwa
wa dhehebu lao wakawalalamikia
wanafunzi wa Yesu, wakisema, “Mbona
mnakula na kunywa pamoja na watoza
ushuru na ‘wenye dhambi’?”
31 Yesu akawajibu, “Wenye afya
hawahitaji tabibu, bali walio wagonjwa.
32 [g]Sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye
dhambi wapate kutubu.”

[a]**5:24** Mt 8:20
[b]**5:26** Mt 9:8
[c]**5:27** Mt 4:19
[d]**5:28** Lk 5:11; Mt 4:19
[e]**5:29** Lk 15:1
[f]**5:30** Mdo 23:9; Mt 9:11
[g]**5:32** Yn 3:17

*Yesu Aulizwa Kuhusu Kufunga*

**(Mathayo 9:14-17; Marko 2:18-22)**

33 [h]Wakamwambia Yesu, “Wanafunzi wa
Yohana na wa Mafarisayo mara kwa mara
hufunga na kuomba, lakini wanafunzi wako
wanaendelea kula na kunywa.”
34 [i]Yesu akawajibu, “Je, mnaweza
kuwafanya wageni wa bwana arusi kufunga
wakati yuko pamoja nao? 35 [j]Lakini wakati
utafika ambapo bwana arusi ataondolewa
kwao. Hapo ndipo watakapofunga.”
36 [k]Yesu akawapa mfano huu,
akawaambia: “Hakuna mtu achanaye kiraka
kutoka kwenye nguo mpya na kukishonea
kwenye nguo iliyochakaa. Akifanya
hivyo, atakuwa amechana nguo mpya,
na kile kiraka hakitalingana na ile nguo
iliyochakaa. 37 [l]Hakuna mtu awekaye divai
mpya kwenye viriba vikuukuu. Akifanya
hivyo, hiyo divai mpya itavipasua hivyo
viriba, nayo yote itamwagika. 38 [m]Divai
mpya lazima iwekwe kwenye viriba vipya.
39 [n]Wala hakuna mtu anayependelea divai
mpya baada ya kunywa divai ya zamani,
bali husema, ‘Ile ya zamani ni nzuri zaidi.’ ”

*Bwana Wa Sabato*

**(Mathayo 12:1-8; Marko 2:23-28)**

6 [o]Ikawa siku moja ya Sabato Yesu alikuwa
akipita katika mashamba ya nafaka, nao
wanafunzi wake wakaanza kuvunja masuke
ya nafaka, wakayafikicha kwa mikono yao
na kula punje zake. 2 [p]Baadhi ya Mafarisayo
wakawauliza, “Mbona mnafanya mambo
yasiyo halali kufanywa siku ya Sabato?”
3 [q]Yesu akawajibu, “Je, ninyi hamjasoma
kamwe alivyofanya Daudi wakati yeye na

[h]**5:33** Lk 7:18; Yn 1:35; 3:25-26; Mt 14:17; Mk 2:18-22
[i]**5:34** Yn 3:29; Mt 14:17; Mk 2:18-22
[j]**5:35** Lk 9:22; 7:22; Mt 14:17; Mk 2:18-22
[k]**5:36** Mt 14:17; Mk 2:18-22; Mt 9:16, 17; Mk 2:21, 22
[l]**5:37** Mt 14:17; Mk 2:18-22
[m]**5:38** Mt 14:17; Mk 2:18-22
[n]**5:39** Mt 14:17; Mk 2:18-22
[o]**6:1** Kum 23:25
[p]**6:2** Mt 12:2
[q]**6:3** 1Sam 21:6

wenzake walikuwa na njaa? 4 [a]Aliingia
ndani ya nyumba ya Mungu, akaichukua
na kuila ile mikate iliyowekwa wakfu,
ambayo ni halali kuliwa na makuhani peke
yao. Naye pia akawapa wenzake.” 5 [b]Yesu
akawaambia, “Mwana wa Adamu ndiye
Bwana wa Sabato.”

*Mtu Aliyepooza Mkono Aponywa*

**(Mathayo 12:9-14; Marko 3:1-6)**

6 [c]Ikawa siku nyingine ya Sabato, Yesu
aliingia ndani ya sinagogi na akawa
anafundisha. Huko palikuwa na mtu ambaye
mkono wake wa kuume ulikuwa umepooza.
7 [d]Mafarisayo na walimu wa sheria
walikuwa wakitafuta sababu ya kumshtaki
Yesu. Kwa hivyo wakawa wanamwangalia
sana ili waone kama ataponya katika siku
ya Sabato. 8 [e]Lakini Yesu alijua mawazo
yao, hivyo akamwambia yule mwenye
mkono uliopooza, “Inuka usimame mbele
ya watu wote.” Hivyo yule mtu akainuka,
akasimama mbele yao wote.

9 Ndipo Yesu akawaambia wale walimu
wa sheria na Mafarisayo, “Nawauliza
ninyi, ni lipi lililo halali siku ya Sabato?
Ni kutenda mema au kutenda mabaya? Ni
kuokoa maisha au kuyaangamiza?”

10 [f]Akawatazama watu wote waliokuwepo,
kisha akamwambia yule aliyepooza mkono,
“Nyoosha mkono wako!” Akaunyoosha na
mkono wake ukaponywa kabisa. 11 [g]Wale
wakuu wakakasirika sana, wakashauriana
wao kwa wao ni nini watakachomtendea
Yesu.

*Yesu Achagua Mitume Kumi Na Wawili*

**(Mathayo 10:1-4; Marko 3:13-19)**

12 [h]Ikawa katika siku hizo Yesu alikwenda
mlimani kuomba, akakesha usiku kucha
akimwomba Mungu. 13 [i]Kulipopambazuka,
akawaita wanafunzi wake, naye akachagua
kumi na wawili, ambao pia aliwaita
mitume: 14 [j]Simoni aliyemwita Petro,
Andrea nduguye, Yakobo, Yohana, Filipo,
Bartholomayo, 15 [k]Mathayo, Tomaso,
Yakobo mwana wa Alfayo, Simoni aliyeitwa
Zelote, 16 Yuda mwana wa Yakobo, na Yuda
Iskariote ambaye alikuwa msaliti.

*Yesu Aponya Wengi*

**(Mathayo 4:23-25)**

17 [l]Akashuka pamoja nao, akasimama
mahali penye uwanja tambarare. Hapo
palikuwa na idadi kubwa ya wanafunzi
wake na umati mkubwa wa watu
kutoka sehemu zote za Uyahudi, kutoka
Yerusalemu, na kutoka pwani ya Tiro na
Sidoni. 18 [m]Walikuwa wamekuja kumsikiliza
na kuponywa magonjwa yao. Wale
waliokuwa wakiteswa na pepo wachafu
akawaponya. 19 [n]Watu wote walikuwa
wanajitahidi kumgusa kwa sababu nguvu
zilikuwa zikimtoka na kuwaponya wote.

*Baraka Na Ole*

**(Mathayo 5:1-12)**

20 [o]Akawatazama wanafunzi wake,
akasema:

“Mmebarikiwa ninyi mlio maskini,
kwa sababu Ufalme wa Mungu ni
wenu.
21 [p]Mmebarikiwa ninyi mlio na njaa
sasa,
kwa sababu mtashibishwa.
Mmebarikiwa ninyi mnaolia sasa,
kwa sababu mtacheka.

---

[a]**6:4** Law 24:5-9
[b]**6:5** Mt 8:20
[c]**6:6** Lk 6:1; Mt 12:9; Mk 3:1; Lk 13:14; 14:3; Yn 9:16
[d]**6:7** Mt 9:4
[e]**6:8** Mt 9:4
[f]**6:10** Mt 13:47
[g]**6:11** Yn 5:18
[h]**6:12** Lk 3:21
[i]**6:13** Mk 6:30
[j]**6:14** Yn 1:42
[k]**6:15** Mt 9:9
[l]**6:17** Mt 11:21; Mk 3:7-8; Mt 4:23; 5:1; Mk 3:7-12
[m]**6:18** Mt 4:23; 5:1; Mk 3:7-12
[n]**6:19** Mt 9:20; 14:36; Mk 5:30; Mt 4:23; 5:1; Mk 3:7-12
[o]**6:20** Mt 25:34
[p]**6:21** Isa 55:1; 61:2-3; Ufu 7:17

22 [a]Mmebarikiwa ninyi, watu
watakapowachukia,
watakapowatenga na kuwatukana
na kulikataa jina lenu kama neno
ovu,
kwa ajili ya Mwana wa Adamu.

23 [b]“Furahini na kurukaruka kwa
shangwe, kwa sababu thawabu yenu ni
kubwa mbinguni, kwa kuwa hivyo ndivyo
baba zao walivyowatenda manabii.

24 [c]“Lakini ole wenu ninyi mlio
matajiri,
kwa sababu mmekwisha kupokea
faraja yenu.
25 [d]Ole wenu ninyi mlioshiba sasa,
maana mtaona njaa.
Ole wenu ninyi mnaocheka sasa,
maana mtaomboleza na kulia.
26 [e]Ole wenu watu watakapowasifu,
kwani ndivyo baba zao
walivyowasifu
manabii wa uongo.

*Wapendeni Adui Zenu*

**(Mathayo 5:38-48)**

27 [f]“Lakini nawaambia ninyi mnaonisikia:
Wapendeni adui zenu. Watendeeni
mema wanaowachukia. 28 [g]Wabarikini
wale wanaowalaani, waombeeni wale
wanaowatendea mabaya. 29 [h]Kama mtu
akikupiga shavu moja, mgeuzie na la pili pia.
Mtu akikunyang’anya koti lako, usimzuie
kuchukua joho pia. 30 [i]Mpe kila akuombaye,
na kama mtu akichukua mali yako usitake
akurudishie. 31 [j]Watendeeni wengine kama
ambavyo mngetaka wawatendee ninyi.
32 [k]“Kama mkiwapenda tu wale
wanaowapenda, mwapata sifa gani?
Hata ‘wenye dhambi’ huwapenda wale
wawapendao. 33 Tena mkiwatendea
mema wale tu wanaowatendea ninyi
mema, mwapata sifa gani? Hata ‘wenye
dhambi’ hufanya vivyo hivyo. 34 [l]Tena
mnapowakopesha wale tu mnaotegemea
wawalipe, mwapata sifa gani? Hata
‘wenye dhambi’ huwakopesha ‘wenye
dhambi’ wenzao wakitarajia kulipwa mali
yao yote. 35 [m]Lakini wapendeni adui zenu,
watendeeni mema, wakopesheni bila
kutegemea kurudishiwa mlichokopesha.
Ndipo thawabu yenu itakapokuwa kubwa,
nanyi mtakuwa wana wa Aliye Juu Sana,
kwa sababu yeye ni mwema kwa watu
wasio na shukrani na kwa wale waovu.
36 [n]Kuweni na huruma, kama Baba yenu
alivyo na huruma.

*Kuwahukumu Wengine*

**(Mathayo 7:1-5)**

37 [o]“Msihukumu, nanyi hamtahukumiwa.
Msilaumu, nanyi hamtalaumiwa. Sameheni,
nanyi mtasamehewa. 38 [p]Wapeni watu
vitu, nanyi mtapewa. Kipimo cha kujaa
na kushindiliwa na kusukwasukwa hata
kumwagika, ndicho watu watakachowapa
vifuani mwenu. Kwa kuwa kipimo kile
mpimacho, ndicho mtakachopimiwa.”
39 [q] Pia akawapa mfano akasema, “Je,
kipofu aweza kumwongoza kipofu? Je,
wote wawili hawatatumbukia shimoni?
40 [r]Mwanafunzi hawezi kumzidi mwalimu
wake, ila yule aliyehitimu aweza kuwa
kama mwalimu wake.
41 [s]“Mbona unatazama kibanzi kilicho

---

[a]**6:22** Yn 9:22; 16:2; 15:21; Isa 51:7; Yn 15:19; 16:2
[b]**6:23** Mt 5:21; 5:12; Mdo 5:41; Kol 1:24; Yak 1:2; Mdo 7:51
[c]**6:24** Yak 5:1; Lk 16:25; Amo 6:1; Yak 5:1; Lk 12:21; Mt 6:2, 5, 16; Lk 16:25
[d]**6:25** Isa 65:13; Mit 14:13; Isa 65:13; Mit 14; 13
[e]**6:26** Mt 7:15; Yn 15:19; 1Yn 4:5
[f]**6:27** Mt 5:44; Rum 12:20; Kut 23:4; Mt 5:44; Lk 6:35; Rum 12:20
[g]**6:28** Lk 23:34; Mdo 7:60
[h]**6:29** Mt 5:39; 1Kor 6:7
[i]**6:30** Kum 15:7-10; Mt 21:36
[j]**6:31** Mt 7:12
[k]**6:32** Mt 5:42-46
[l]**6:34** Mt 5:42
[m]**6:35** Rum 8:14; Mk 5:7
[n]**6:36** Yak 2:13; 1Pet 1:17; 1Yn 3:1
[o]**6:37** Mt 7:1; 6:14
[p]**6:38** Za 79:12; Isa 65:6-7; Mk 4:24
[q]**6:39** Mt 15:14
[r]**6:40** Mt 10:24; Yn 3:16
[s]**6:41** Mt 7:3

ndani ya jicho la ndugu yako, wala huoni
boriti iliyo ndani ya jicho lako mwenyewe?
42 [a]Utawezaje kumwambia ndugu yako,
'Ndugu yangu, acha nitoe kibanzi kilicho
ndani ya jicho lako,' wakati wewe
mwenyewe huoni boriti iliyo ndani ya jicho
lako? Ewe mnafiki, ondoa boriti ndani ya
jicho lako kwanza, ndipo utaweza kuona
dhahiri jinsi ya kuondoa kibanzi kilicho
ndani ya jicho la ndugu yako.

*Mti Na Mazao Yake*

**(Mathayo 7:16-20; Marko 12:33-35)**

43 [b]"Hakuna mti mzuri uzaao matunda
mabaya, wala hakuna mti mbaya uzaao
matunda mazuri. 44 [c]Kila mti hujulikana
kwa matunda yake. Kwa maana watu
hawachumi tini kwenye miiba, wala
zabibu kwenye michongoma. 45 [d]Vivyo
hivyo mtu mwema hutoa mambo mema
kutoka kwenye hazina ya moyo wake,
naye mtu mwovu hutoa mambo maovu
kutoka kwenye hazina ya moyo wake. Kwa
kuwa mtu hunena kwa kinywa chake yale
yaliyoujaza moyo wake.

*Mjenzi Mwenye Busara Na Mjenzi Mpumbavu*

**(Mathayo 7:24-27)**

46 [e]"Kwa nini mnaniita, 'Bwana,
Bwana,' nanyi hamfanyi ninayowaambia?
47 [f]Nitawaonyesha jinsi alivyo mtu yule
anayekuja kwangu na kusikia maneno
yangu na kuyatenda. 48 Yeye ni kama
mtu aliyejenga nyumba, akachimba chini
sana, na kuweka msingi kwenye mwamba.
Mafuriko yalipokuja, maji ya ghafula
yaliipiga ile nyumba, lakini haikutikisika,
kwa sababu ilikuwa imejengwa vizuri.
49 Lakini yeye anayesikia maneno yangu
wala asiyatende, ni kama mtu aliyejenga
nyumba juu ya ardhi bila kuweka msingi.
Mafuriko yalipoikumba nyumba ile,
ikaanguka mara na kubomoka kabisa."

[a]**6:42** Mt 18:17
[b]**6:43** Mt 7:16, 17
[c]**6:44** Mt 12:33
[d]**6:45** Mt 4:23; Mk 7:20
[e]**6:46** Mal 1:6; Mt 7:21
[f]**6:47** Lk 11:28; Yak 1:22-25; Mt 8:9-13

*Yesu Amponya Mtumishi Wa Jemadari*

**(Mathayo 8:5-13)**

7 [g]Baada ya Yesu kumaliza kusema haya
yote watu wakiwa wanamsikiliza,
akaingia Kapernaumu. 2 [h]Mtumishi wa
jemadari mmoja wa Kirumi, ambaye
bwana wake alimthamini sana, alikuwa
mgonjwa sana karibu kufa. 3 Jemadari
huyo aliposikia habari za Yesu, aliwatuma
wazee wa Kiyahudi kwake, wakamwomba
aje kumponya mtumishi wa huyo
jemadari. 4 Wale wazee walipofika kwa
Yesu, wakamsihi sana amsaidie yule
jemadari wakisema, "Mtu huyu anastahili
wewe umfanyie jambo hili, 5 kwa sababu
analipenda taifa letu tena ametujengea
sinagogi." 6 Hivyo Yesu akaongozana
nao, lakini alipokuwa hayuko mbali
na nyumbani, yule jemadari akatuma
rafiki zake kumwambia Yesu, "Bwana,
usijisumbue, kwani mimi sistahili wewe
kuingia chini ya dari yangu. 7 [i]Ndiyo
maana sikujiona hata ninastahili kuja
kwako wewe. Lakini sema neno tu, naye
mtumishi wangu atapona. 8 Kwa kuwa mimi
mwenyewe ni mtu niliyewekwa chini ya
mamlaka, nikiwa na askari chini yangu.
Nikimwambia huyu, 'Nenda,' yeye huenda;
na mwingine nikimwambia, 'Njoo,' yeye
huja. Nikimwambia mtumishi wangu,
'Fanya hivi,' yeye hufanya."
9 Yesu aliposikia maneno haya,
alishangazwa naye sana. Akaugeukia
ule umati wa watu uliokuwa unamfuata,
akawaambia, "Sijaona imani kubwa
namna hii hata katika Israeli." 10 Nao
wale watu waliokuwa wametumwa kwa
Yesu waliporudi nyumbani walimkuta yule
mtumishi amepona.

*Yesu Amfufua Mwana Wa Mjane*

11 Baadaye kidogo, Yesu alikwenda
katika mji mmoja ulioitwa Naini. Nao
wanafunzi wake na umati mkubwa wa watu
walikwenda pamoja naye. 12 [j]Alipokaribia
lango la mji, alikutana na watu waliokuwa

[g]**7:1** Mt 7:28
[h]**7:2** Yn 4:47
[i]**7:7** Za 107:20
[j]**7:12** Lk 8:42; 1Fal 17:17

wamebeba maiti wakitoka nje ya mji.
Huyu aliyekufa alikuwa mwana pekee wa
mwanamke mjane. Umati mkubwa wa
watu wa mji ule ulikuwa pamoja na huyo
mwanamke. 13 [a]Bwana Yesu alipomwona
yule mjane, moyo wake ulimhurumia,
akamwambia, "Usilie."
14 [b]Kisha akasogea mbele akaligusa lile
jeneza na wale waliokuwa wamelibeba
wakasimama kimya. Akasema, "Kijana,
nakuambia inuka." 15 [c]Yule aliyekuwa
amekufa akaketi akaanza kuongea, naye
Yesu akamkabidhi kwa mama yake.
16 [d]Watu wote wakajawa na hofu
ya Mungu, nao wakamtukuza Mungu
wakisema, "Nabii mkuu ametokea miongoni
mwetu, Mungu amekuja kuwakomboa
watu wake." 17 [e]Habari hizi za mambo
aliyoyafanya Yesu zikaenea Uyahudi wote
na sehemu zote za jirani.

*Yesu Na Yohana Mbatizaji*

**(Mathayo 11:2-19)**

18 [f]Wanafunzi wa Yohana Mbatizaji
wakamweleza Yohana mambo haya yote.
Hivyo Yohana akawaita wanafunzi wake
wawili 19 [g]na kuwatuma kwa Bwana ili
kumuuliza, "Wewe ndiye yule aliyekuwa
aje, au tumngojee mwingine?"
20 Wale watu walipofika kwa Yesu
wakamwambia, "Yohana Mbatizaji
ametutuma tukuulize, 'Wewe ndiye yule
aliyekuwa aje, au tumngojee mwingine?' "
21 [h]Wakati huo huo, Yesu aliwaponya
wengi waliokuwa na magonjwa, maradhi
na pepo wachafu, na pia akawafungua
vipofu wengi macho wakapata kuona.
22 [i]Hivyo akawajibu wale wajumbe, "Rudini
mkamwambie Yohana yote mnayoyaona na
kuyasikia: Vipofu wanapata kuona, viwete
wanatembea, wenye ukoma wanatakaswa,
viziwi wanasikia, wafu wanafufuliwa na
maskini wanahubiriwa habari njema.
23 Amebarikiwa mtu yule asiyechukizwa
na mimi."
24 [j]Wajumbe wa Yohana walipoondoka,
Yesu akaanza kusema na makutano
kuhusu Yohana Mbatizaji. Akawauliza,
"Mlipokwenda kule nyikani, mlikwenda
kuona nini? Je, ni unyasi ukipeperushwa
na upepo? 25 Kama sivyo, mlikwenda
kuona nini basi? Mtu aliyevaa mavazi ya
kifahari? La hasha, watu wanaovaa mavazi
ya kifahari na kuishi maisha ya anasa wako
katika majumba ya kifalme. 26 [k]Lakini
mlikwenda kuona nini? Mlikwenda
kumwona nabii? Naam, nawaambia, yeye
ni zaidi ya nabii. 27 [l]Huyu ndiye ambaye
habari zake zimeandikwa:

" 'Tazama, nitamtuma mjumbe
wangu mbele yako,
atakayetengeneza njia mbele
yako.'

28 [m]Nawaambia, miongoni mwa wale
waliozaliwa na wanawake, hakuna aliye
mkuu kuliko Yohana. Lakini yeye aliye
mdogo kabisa katika Ufalme wa Mungu ni
mkuu kuliko Yohana."
29 [n](Watu wote hata watoza ushuru
waliposikia maneno ya Yesu, walikubali
kwamba mpango wa Mungu ni haki,
maana walikuwa wamebatizwa na Yohana.
30 [o]Lakini Mafarisayo na wataalamu wa
sheria walikataa mpango wa Mungu kwao
kwa kutokubali kubatizwa na Yohana.)
31 Yesu akawauliza, "Niwafananishe na
nini watu wa kizazi hiki? Wanafanana
na nini? 32 Wao ni kama watoto waliokaa
sokoni wakiitana wao kwa wao, wakisema:

" 'Tuliwapigia filimbi,
lakini hamkucheza;
tuliwaimbia nyimbo za maombolezo,
lakini hamkulia.'

[a]**7:13** Lk 24:34; Yn 11:2
[b]**7:14** Yn 11:43; Mdo 9:40
[c]**7:15** 1Fal 17:23; 2Fal 4:36
[d]**7:16** Lk 1:65-68; Mt 21:11; 9:8
[e]**7:17** Mt 9:26
[f]**7:18** Mt 3:1; Lk 5:33
[g]**7:19** Za 40:7; 118:26; Mal 3:1; Dan 9:26
[h]**7:21** Mt 4:23
[i]**7:22** Isa 61:1-2; Lk 4:18-19
[j]**7:24** Mt 11:7
[k]**7:26** Mt 11:9-10
[l]**7:27** Mal 3:1
[m]**7:28** Mt 3:2
[n]**7:29** Mt 21:32; Mk 1:5; Lk 3:12
[o]**7:30** Mt 22:25

33 [a]Kwa maana Yohana Mbatizaji alikuja,
alikuwa hali mkate wala hanywi divai,
nanyi mkasema, ‘Yeye ana pepo mchafu.’
34 [b]Mwana wa Adamu alikuja akila na
kunywa, nanyi mnasema: ‘Tazameni huyu
mlafi na mlevi, rafiki wa watoza ushuru
na “wenye dhambi.” ’ 35 [c]Nayo hekima
huthibitishwa kuwa kweli na watoto wake
wote.”

*Yesu Apakwa Mafuta Na Mwanamke Mwenye Dhambi*

36 [d]Basi Farisayo mmoja alimwalika Yesu
nyumbani kwake kwa chakula. Hivyo Yesu
akaenda nyumbani mwa yule Farisayo na
kukaa katika nafasi yake mezani. 37 Naye
mwanamke mmoja kwenye ule mji, ambaye
alikuwa mwenye dhambi, alipojua kwamba
Yesu alikuwa akila chakula nyumbani kwa
yule Farisayo, akaleta chupa ya marhamu
yenye manukato. 38 [e]Yule mwanamke
akasimama nyuma ya miguu ya Yesu akilia.
Akailowanisha miguu yake kwa machozi
yake, kisha akaifuta kwa nywele zake,
akaibusu na kuimiminia manukato.

39 [f]Yule Farisayo aliyemwalika Yesu
alipoona yanayotendeka, akawaza moyoni
mwake, “Kama huyu mtu angekuwa nabii,
angejua kwamba ni nani anayemgusa, na
kwamba yeye ni mwanamke wa namna
gani, na ya kuwa huyu mwanamke ni
mwenye dhambi.”

40 Yesu akanena akamwambia, “Simoni,
nina jambo la kukuambia.”

Simoni akajibu, “Mwalimu, sema.”

41 “Palikuwa na mtu mmoja
aliyewakopesha watu wawili fedha: Mmoja
alidaiwa dinari 500[g] na mwingine dinari
hamsini. 42 Wote wawili walipokuwa
hawawezi kulipa, aliyafuta madeni
yao wote wawili. Sasa ni yupi kati yao
atakayempenda yule aliyewasamehe zaidi?”

43 Simoni akajibu, “Nadhani ni yule
aliyesamehewa deni kubwa zaidi.”

Naye Yesu akamwambia, “Umehukumu
kwa usahihi.”

44 [h]Kisha akamgeukia yule mwanamke,
akamwambia Simoni, “Je, unamwona
mwanamke huyu? Nilipoingia nyumbani
mwako, hukunipa maji ya kunawa miguu
yangu, lakini huyu ameninawisha miguu
kwa machozi yake, na kunifuta kwa nywele
zake. 45 [i]Hukunisalimu kwa busu, lakini
huyu mwanamke hajaacha kuibusu miguu
yangu tangu nilipoingia. 46 [j]Hukunipaka
mafuta kichwani mwangu, lakini yeye
ameipaka miguu yangu manukato. 47 [k]Kwa
hiyo, nakuambia, dhambi zake zilizokuwa
nyingi zimesamehewa, kwani ameonyesha
upendo mwingi. Lakini yule aliyesamehewa
kidogo, hupenda kidogo.”

48 [l]Kisha akamwambia yule mwanamke,
“Dhambi zako zimesamehewa.”

49 [m]Lakini wale waliokuwa wameketi
pamoja naye chakulani wakaanza
kusemezana wao kwa wao, “Huyu ni nani
ambaye hata anasamehe dhambi?”

50 [n]Yesu akamwambia yule mwanamke,
“Imani yako imekuokoa; nenda kwa amani.”

*Mfano Wa Mpanzi*

**(Mathayo 13:1-9; Marko 4:1-9)**

8 [o]Baada ya haya Yesu alikwenda, akawa
anazunguka katika miji na vijiji akihubiri
habari njema za Ufalme wa Mungu. Wale
wanafunzi wake kumi na wawili walikuwa
pamoja naye, 2 [p]pia baadhi ya wanawake
waliokuwa wametolewa pepo wachafu na
kuponywa magonjwa. Miongoni mwao
alikuwepo Maria Magdalene, aliyetolewa
pepo wachafu saba; 3 [q]Yoana mkewe
Kuza, msimamizi wa nyumba ya watu

---

[a]**7:33** Lk 1:15
[b]**7:34** Lk 5:29-30; 15:1-2
[c]**7:35** Mt 11:6
[d]**7:36** Mt 26:6; Mk 14:3; Yn 11:2; Lk 11:37
[e]**7:38** Mt 26:7-13; Yn 12:3-8
[f]**7:39** Mt 21:11
[g]41 Dinari 500 ni sawa na mshahara wa kibarua wa siku mia tano.
[h]**7:44** Amu 19:21; 1Tim 5:10
[i]**7:45** Lk 22:47-48; Rum 16:16
[j]**7:46** Za 23:5; Mhu 9:8
[k]**7:47** 1Tim 1:14
[l]**7:48** Mt 9:2
[m]**7:49** Mt 9:3; Mk 2:7
[n]**7:50** Mt 9:22; Mk 5:34; Mdo 15:33
[o]**8:1** Mt 4:23
[p]**8:2** Mt 27:55-56
[q]**8:3** Mt 14:1

wa nyumbani mwa Herode; Susana; na
wengine wengi waliokuwa wakimhudumia
kwa mali zao.
4 [a][b]Umati mkubwa wa watu ulipokuwa
ukija kwa Yesu kutoka kila mji,
akawaambia mfano huu: 5 “Mpanzi alitoka
kwenda kupanda mbegu zake. Alipokuwa
akitawanya mbegu, nyingine zilianguka
kando ya njia; zikakanyagwa, nao ndege
wa angani wakazila. 6 Mbegu nyingine
zilianguka penye miamba, nazo zilipoota,
hiyo mimea ikakauka kwa kukosa unyevu.
7 Nazo mbegu nyingine zilianguka kwenye
miiba, nayo ile miiba ikakua pamoja nazo,
na kuisonga hiyo mimea. 8 [c]Mbegu nyingine
zilianguka kwenye udongo mzuri. Zikaota
na kuzaa mara mia moja zaidi ya mbegu
alizopanda.”

Baada ya kusema haya, Yesu akapaza sauti, akasema, “Mwenye masikio ya kusikia, na asikie.”

9 [d]Wanafunzi wake wakamuuliza maana
ya mfano huo. 10 [e]Naye akasema, “Ninyi
mmepewa kufahamu siri za Ufalme wa
Mungu, lakini kwa wengine nazungumza
kwa mifano, ili,

“ ‘ingawa wanatazama, wasione;
ingawa wanasikiliza, wasielewe.’

11 [f]“Maana ya mfano huu ni hii: Mbegu ni
neno la Mungu. 12 Zile zilizoanguka kando
ya njia ni wale ambao husikia neno, naye
ibilisi anakuja na kuliondoa neno kutoka
mioyoni mwao, ili wasije wakaamini na
kuokoka. 13 [g]Zile mbegu zilizoanguka
kwenye mwamba ni wale ambao hulipokea
neno kwa furaha wanapolisikia, lakini
hawana mizizi. Wanaamini kwa muda
mfupi, lakini wakati wa kujaribiwa huiacha
imani. 14 [h]Zile mbegu zilizoanguka kwenye
miiba ni mfano wa wale wanaosikia, lakini
wanapoendelea husongwa na masumbufu
ya maisha haya, utajiri na anasa, nao
hawakui. 15 [i]Lakini zile mbegu zilizoanguka
kwenye udongo mzuri ni mfano wa wale ambao hulisikia neno la Mungu na kulishika kwa moyo mnyofu wa utiifu, nao kwa kuvumilia kwingi huzaa matunda.

*Mfano Wa Taa*

**(Marko 4:21-25)**

16 [j]“Hakuna mtu awashaye taa na kuificha
ndani ya gudulia au kuiweka mvunguni
mwa kitanda. Badala yake, huiweka juu
ya kinara, ili wale waingiao ndani waone
mwanga. 17 [k]Kwa maana hakuna jambo lolote
lililofichika ambalo halitafichuliwa, wala
lolote lililositirika ambalo halitajulikana
na kuwekwa wazi. 18 [l]Kwa hiyo, kuweni
waangalifu mnavyosikia. Kwa maana yeyote aliye na kitu atapewa zaidi. Lakini yule asiye na kitu, hata kile anachodhani anacho atanyang’anywa.”

*Mama Yake Yesu Na Ndugu Zake*

**(Mathayo 12:46-50; Marko 3:31-35)**

19 [m]Wakati mmoja mama yake Yesu na
ndugu zake walikuja kumwona, lakini
hawakuweza kumfikia kwa sababu ya
msongamano wa watu. 20 [n]Mtu mmoja
akamwambia, “Mama yako na ndugu zako wako nje wanataka kukuona.”
21 [o]Yesu akamjibu, “Mama yangu na ndugu zangu ni wale wote wanaolisikia neno la Mungu na kulifanya.”

*Yesu Atuliza Dhoruba*

**(Mathayo 8:23-27; Marko 4:35-41)**

22 [p][q]Siku moja Yesu alipanda ndani ya mashua pamoja na wanafunzi wake, akawaambia, “Tuvukeni twende mpaka ng’ambo ya ziwa.” Nao wakaondoka.

[a]**8:4** Mt 13:2; Mk 4:1
[b]**8:4** Mt 13:23; Kum 4:1-20
[c]**8:8** Mt 11:15
[d]**8:9** Mt 13:10; Mk 4:10
[e]**8:10** Mt 13:11; Isa 6:9; Mt 13:13-14
[f]**8:11** Ebr 4:12
[g]**8:13** Mt 11:6
[h]**8:14** Mt 19:23; 1Tim 6:9-17
[i]**8:15** Mdo 16:14; Ebr 10:36; Ufu 3:10
[j]**8:16** Mt 5:15; Mk 4:21
[k]**8:17** Mt 10:26; Mk 4:22
[l]**8:18** Mt 13:12; 25:29
[m]**8:19** Mt 12:46; Mk 3:31
[n]**8:20** Yn 7:5
[o]**8:21** Lk 11:28; Yn 14:21
[p]**8:22** Mt 8:23; Mk 4:35
[q]**8:22** Mt 8:18; 23:27; Mk 4:35-41

23 Hivyo walipokuwa wakienda, akalala
usingizi. Dhoruba kali ikatokea mle
ziwani, hata mashua ikawa inajaa maji,
nao walikuwa katika hatari kubwa.
24 [a]Wanafunzi wake wakamwendea na
kumwamsha, wakisema, "Bwana, Bwana,
tunaangamia!"

Yeye akaamka, akaukemea ule upepo
na yale mawimbi; dhoruba ikakoma, nako
kukawa shwari. 25 Akawauliza wanafunzi
wake, "Imani yenu iko wapi?"

Kwa woga na mshangao wakaulizana,
"Huyu ni nani, ambaye anaamuru hata
upepo na maji, navyo vikamtii?"

*Yesu Amponya Mtu Mwenye Pepo Mchafu*

**(Mathayo 8:28-34; Marko 5:1-20)**

26 [bc]Basi wakafika katika nchi ya Wagerasi,
ambayo iko upande wa pili wa ziwa kutoka
Galilaya. 27 Yesu aliposhuka kutoka mashua
na kukanyaga ufuoni, alikutana na mtu
mmoja wa mji ule aliyekuwa amepagawa
na pepo mchafu, naye kwa muda mrefu
alikuwa havai nguo wala kuishi nyumbani,
bali aliishi makaburini. 28 [d]Alipomwona
Yesu, alipiga kelele, akajitupa chini mbele
yake na kusema kwa sauti kuu, "Una nini
nami, Yesu, Mwana wa Mungu Aliye Juu
Sana? Nakuomba, usinitese!" 29 Wakati
huo Yesu alikuwa amemwamuru yule pepo
mchafu amtoke huyo mtu. Mara nyingi
huyo pepo mchafu alimpagaa, na hata
alipofungwa kwa minyororo mikono na
miguu na kuwekwa chini ya ulinzi, alikata
hiyo minyororo na kupelekwa na huyo pepo
mchafu kwenda nyikani.

30 Yesu akamuuliza, "Jina lako ni nani?"

Akamjibu, "Legioni,"[e] kwa kuwa alikuwa
ameingiwa na pepo wachafu wengi mno.
31 [f]Wale pepo wachafu wakamsihi sana
asiwaamuru kwenda katika Shimo.[g]

32 Palikuwa na kundi kubwa la nguruwe
hapo likilisha kando ya kilima. Wale pepo
wachafu wakamsihi Yesu awaruhusu
wawaingie hao nguruwe, naye akawaruhusu.
33 [h]Wale pepo wachafu walipomtoka yule
mtu, wakawaingia wale nguruwe, nalo
kundi lote likateremkia gengeni kwa kasi,
likatumbukia ziwani na kuzama.

34 Wale watu waliokuwa wakichunga lile
kundi la nguruwe walipoona yaliyotukia,
wakakimbia, wakaeneza habari hizi mjini
na mashambani. 35 [i]Nao watu wakatoka
kwenda kujionea wenyewe yaliyotukia.
Walipofika hapo alipokuwa Yesu,
wakamkuta yule mtu aliyetokwa na pepo
wachafu amekaa karibu na Yesu, akiwa
amevaa nguo na mwenye akili timamu!
Wakaogopa. 36 [j]Wale walioyaona mambo
hayo wakawaeleza watu wengine jinsi
yule mtu aliyekuwa amepagawa na pepo
wachafu alivyoponywa. 37 [k]Ndipo watu
wote wa nchi ile ya Wagerasi wakamwomba
Yesu aondoke kwao, kwa sababu walikuwa
wamejawa na hofu. Basi akaingia katika
mashua, akaondoka zake.

38 [l]Yule mtu aliyetokwa na pepo wachafu
akamsihi Yesu afuatane naye, lakini
Yesu akamuaga, akamwambia: 39 "Rudi
nyumbani ukawaeleze mambo makuu
Mungu aliyokutendea." Kwa hiyo yule
mtu akaenda, akatangaza katika mji wote
mambo makuu ambayo Yesu alimtendea.

*Msichana Afufuliwa, Na Mwanamke Aponywa*

**(Mathayo 9:18-26; Marko 5:21-43)**

40 [m]Basi Yesu aliporudi, umati mkubwa
wa watu ukampokea kwa furaha, kwani
walikuwa wakimngojea. 41 [n]Kisha mtu
mmoja, jina lake Yairo, aliyekuwa kiongozi
wa sinagogi, akaja na kuanguka miguuni
mwa Yesu, akimwomba afike nyumbani
kwake, 42 [o]kwa kuwa binti yake wa pekee,

---

[a]**8:24** Lk 5:5; 4:35-39, 41; Za 107:29; Yn 1:15
[b]**8:26** Mt 8:28; Mk 5:1
[c]**8:26** Mt 8:28-34; Mk 5:1-20
[d]**8:28** Mt 8:29; Mk 5:7
[e]30 Legioni maana yake ni Jeshi.
[f]**8:31** Ufu 17:8; 20:1-3
[g]31 Shimo hapa ina maana Abyss (shimo lisilo na mwisho), yaani Kuzimu; kwa Kiebrania ni Sheol.
[h]**8:33** Lk 8:22-23
[i]**8:35** Lk 10:39
[j]**8:36** Mt 4:24
[k]**8:37** Mdo 16:39
[l]**8:38** Mk 5:18
[m]**8:40** Mt 9:18-26; Mk 5:21-43
[n]**8:41** Mk 5:22
[o]**8:42** Lk 7:12

mwenye umri wa miaka kumi na miwili,
alikuwa anakufa.

Yesu alipokuwa akienda, umati wa watu
ukamsonga sana. [43] [a]Katika umati huo
palikuwa na mwanamke mmoja aliyekuwa
na tatizo la kutokwa damu kwa muda
wa miaka kumi na miwili. Tena alikuwa
amegharimia yote aliyokuwa nayo kwa
ajili ya matibabu, wala hakuna yeyote
aliyeweza kumponya. [44] [b]Huyo mwanamke
akaja kwa nyuma ya Yesu na kugusa upindo
wa vazi lake. Mara kutokwa damu kwake
kukakoma.

[45] [c]Yesu akauliza, "Ni nani aliyenigusa?"

Watu wote walipokana, Petro akasema,
"Bwana, huu umati wa watu unakusonga
na kukusukuma kila upande."

[46] [d]Lakini Yesu akasema, "Kuna mtu
aliyenigusa, kwa maana nimetambua kuwa
nguvu zimenitoka."

[47] Yule mwanamke alipofahamu ya
kuwa hawezi kuendelea kujificha, alikuja
akitetemeka, akaanguka miguuni mwa
Yesu. Akaeleza mbele ya watu wote kwa
nini alimgusa na jinsi alivyoponywa mara.
[48] [e]Basi Yesu akamwambia, "Binti, imani
yako imekuponya. Nenda kwa amani."

[49] [f]Yesu alipokuwa bado anasema, akaja
mtumishi kutoka nyumbani kwa Yairo,
yule kiongozi wa sinagogi, kumwambia,
"Binti yako amekwisha kufa. Usiendelee
kumsumbua Mwalimu."

[50] Yesu aliposikia jambo hili, akamwambia
Yairo, "Usiogope. Amini tu, naye binti yako
atapona."

[51] [g]Walipofika nyumbani kwa Yairo,
hakumruhusu mtu yeyote aingie ndani
naye isipokuwa Petro, Yakobo na Yohana,
pamoja na baba na mama wa yule binti.
[52] [h]Wakati ule ule watu wote walikuwa
wakilia na kuomboleza kwa ajili ya huyo
binti. Yesu akawaambia, "Acheni kulia.
Huyu binti hajafa, ila amelala."

[53] Wao wakamcheka kwa dharau, wakijua
kuwa amekwisha kufa. [54] [i]Yesu akamshika
yule binti mkono na kuita, "Binti, amka!"
[55] Roho yake ikamrudia, naye akainuka
mara moja. Akaamuru apewe kitu cha
kula. [56] [j]Wazazi wake wakastaajabu sana,
lakini Yesu akawakataza wasimwambie mtu
yeyote juu ya yale yaliyotukia.

### *Yesu Awatuma Wale Kumi Na Wawili*

**(Mathayo 10:5-15; Marko 6:7-13)**

9 [k]Yesu kisha akawaita wale kumi na wawili
pamoja, akawapa mamlaka na uwezo
wa kutoa pepo wachafu wote na kuponya
magonjwa yote, [2] [l]kisha akawatuma
waende wakahubiri Ufalme wa Mungu
na kuponya wagonjwa. [3] [m]Akawaagiza
akisema, "Msichukue chochote safarini:
sio fimbo, wala mkoba, wala mkate, wala
fedha, hata msichukue kanzu ya ziada.
[4] [n]Katika nyumba yoyote mwingiayo,
kaeni humo hadi mtakapoondoka katika
mji huo. [5] [o]Kama watu wasipowakaribisha,
mnapoondoka katika mji wao, kung'uteni
mavumbi kutoka kwenye miguu yenu ili
kuwa ushuhuda dhidi yao." [6] [p]Hivyo wale
wanafunzi wakaondoka wakaenda kutoka
kijiji hadi kijiji, wakihubiri habari njema
na kuponya wagonjwa kila mahali.

### *Herode Afadhaika*

**(Mathayo 14:1-12; Marko 6:14-29)**

[7] [q]Basi Mfalme Herode, mtawala
wa Galilaya, alisikia habari za yote
yaliyotendeka. Naye akafadhaika, kwa kuwa
baadhi ya watu walikuwa wakisema Yohana
Mbatizaji amefufuliwa kutoka kwa wafu.
[8] [r]Wengine wakasema Eliya amewatokea,

[a]**8:43** Law 15:25-30
[b]**8:44** Mt 9:20
[c]**8:45** Lk 5:5
[d]**8:46** Mt 14:36; Mk 3:10; Lk 5:17; 6:19
[e]**8:48** Mt 9:22; Mdo 15:33
[f]**8:49** Lk 8:41
[g]**8:51** Mt 4:21
[h]**8:52** Lk 23:27; Mt 9; 24; Yn 11:11-13
[i]**8:54** Lk 7:14
[j]**8:56** Mt 8:4
[k]**9:1** Mt 10:1; 4:23; Lk 5:17
[l]**9:2** Mt 3:2
[m]**9:3** Lk 10:4; 22:35
[n]**9:4** Mt 10:11; Mk 6:10
[o]**9:5** Lk 10:14
[p]**9:6** Mk 6:12
[q]**9:7** Mt 3:1; 14:1
[r]**9:8** Mt 11:14; Yn 1:21

na wengine wakasema kwamba mmoja
wa manabii wa kale amefufuka. 9 [a]Herode
akasema, "Yohana nilimkata kichwa. Lakini ni nani huyu ambaye ninasikia mambo kama haya kumhusu?" Akatamani sana kumwona.

*Yesu Awalisha Wanaume 5,000*

**(Mathayo 14:13-21; Marko 6:30-44; Yohana 6:1-14)**

10 [b]Mitume wake waliporudi, wakamweleza Yesu yote waliyofanya. Akawachukua, akaenda nao faraghani
mpaka mji uitwao Bethsaida. 11 [c]Lakini
umati wa watu ukafahamu alikokwenda, ukamfuata. Akawakaribisha na kunena nao kuhusu Ufalme wa Mungu na kuwaponya wale wote waliokuwa wanahitaji uponyaji.
12 [d]Ilipokaribia jioni, wale mitume kumi na wawili wakaenda kwa Yesu na kumwambia, "Waage makutano ili waende vijijini jirani na mashambani, ili wapate chakula na mahali pa kulala, kwa maana hapa tuko nyikani."
13 Yesu akawajibu, "Ninyi wapeni chakula."

Nao wakajibu, "Hatuna zaidi ya mikate mitano na samaki wawili. Labda twende tukanunue chakula cha kuwatosha watu
hawa wote." 14 Walikuwako wanaume
wapatao 5,000.

Yesu akawaambia wanafunzi wake, "Waketisheni katika makundi ya watu
hamsini hamsini." 15 Wanafunzi wakafanya
hivyo, wakawaketisha wote. 16 [e]Yesu
akaichukua ile mikate mitano na wale samaki wawili, akatazama mbinguni, akavibariki na kuvimega. Kisha akawapa
wanafunzi ili wawagawie watu. 17 Wote
wakala, wakashiba. Nao wanafunzi wakakusanya vipande vilivyosalia, wakajaza vikapu kumi na viwili.

*Petro Amkiri Yesu Kuwa Ndiye Kristo*

**(Mathayo 16:13-19; Marko 8:27-29)**

18 [f]Wakati mmoja, Yesu alipokuwa akiomba faraghani, nao wanafunzi wake wakiwa pamoja naye, akawauliza, "Watu husema mimi ni nani?"
19 [g]Wakamjibu, "Baadhi husema wewe ni Yohana Mbatizaji, wengine husema ni Eliya, na bado wengine husema kwamba ni mmoja wa manabii wa kale amefufuka kutoka kwa wafu."
20 [h]Kisha akawauliza, "Je, ninyi mnasema mimi ni nani?"

Petro akajibu, "Wewe ndiwe Kristo[i] wa Mungu."
21 [j]Yesu akawakataza wasimwambie
mtu yeyote jambo hilo. 22 [k]Yesu akasema,
"Imempasa Mwana wa Adamu kupata mateso mengi na kukataliwa na wazee, viongozi wa makuhani, na walimu wa sheria, na itampasa auawe, lakini siku ya tatu kufufuliwa kutoka mauti."
23 [l]Kisha akawaambia wote, "Mtu yeyote akitaka kunifuata, ni lazima ajikane mwenyewe, auchukue msalaba
wake kila siku, anifuate. 24 [m]Kwa maana
yeyote anayetaka kuyaokoa maisha yake atayapoteza, lakini yeyote atakayeyapoteza maisha yake kwa ajili yangu atayaokoa.
25 [n]Je, itamfaidi nini mtu kuupata ulimwengu wote, lakini akapoteza au kuangamiza nafsi
yake? 26 [o]Mtu yeyote akinionea aibu mimi
na maneno yangu, Mwana wa Adamu naye atamwonea aibu atakapokuja katika utukufu wake na katika utukufu wa Baba, pamoja na
malaika watakatifu. 27 [p]Amin, nawaambia,
wako baadhi ya watu waliosimama hapa

---

[a]**9:9** Lk 23:8
[b]**9:10** Mk 6:30; Mt 11:21
[c]**9:11** Lk 9:2
[d]**9:12** Mt 14:15; Mk 6:35; Yn 6:1, 5
[e]**9:16** Mt 14:19
[f]**9:18** Lk 3:21
[g]**9:19** Mt 14:2; Lk 9:7; 8
[h]**9:20** Yn 1:49; 11:27
[i]20 *Kristo* maana yake ni *Masiya*, yaani *Aliyetiwa mafuta.*
[j]**9:21** Mt 16:20; Mk 8:30
[k]**9:22** Mt 8:20; 16:21; 27:1-2; Mdo 2:23; 3:13
[l]**9:23** Mt 10:38; Lk 14:27
[m]**9:24** Yn 12:25
[n]**9:25** Mt 16:26; Mk 8:36
[o]**9:26** 2Tim 2:12; Mt 16; 27; 10:33
[p]**9:27** Mt 16:28; Mk 9:1

ambao hawataonja mauti kabla ya kuuona
Ufalme wa Mungu.”

*Bwana Yesu Abadilika Sura*

**(Mathayo 17:1-8; Marko 9:2-8)**

28 [a]Yapata siku nane baada ya Yesu
kusema hayo, aliwachukua Petro,
Yakobo na Yohana, akaenda nao mlimani
kuomba. 29 Alipokuwa akiomba, sura ya
uso wake ikabadilika, nayo mavazi yake
yakametameta kama mwanga wa umeme
wa radi. 30 Ghafula wakawaona watu
wawili, ndio Mose na Eliya, wakizungumza
naye. 31 [b]Walionekana katika utukufu
wakizungumza na Yesu kuhusu kifo chake
ambacho kingetokea huko Yerusalemu.
32 [c]Petro na wenzake walikuwa wamelala
usingizi mzito. Walipoamka, wakaona
utukufu wa Yesu na wale watu wawili
waliokuwa wamesimama pamoja naye.
33 [d]Mose na Eliya walipokuwa wanaondoka,
Petro akamwambia Yesu, “Bwana, ni vizuri
tukae hapa! Tutajenga vibanda vitatu:
kimoja chako, kingine cha Mose na kingine
cha Eliya.” Lakini Petro alikuwa hajui
asemacho.

34 Alipokuwa bado anazungumza,
pakatokea wingu, likawafunika, nao
wakaogopa walipoingia mle kwenye
wingu. 35 [e]Sauti ikatoka kwenye lile wingu
ikisema, “Huyu ni Mwanangu mpendwa,
niliyemchagua. Msikieni yeye.” 36 [f]Baada
ya sauti hiyo kusema, walimkuta Yesu
akiwa peke yake. Wale wanafunzi
wakalihifadhi jambo hili, wala kwa wakati
huo hawakumwambia mtu yeyote yale
waliyokuwa wameyaona.

*Kuponywa Kwa Kijana Mwenye Pepo Mchafu*

**(Mathayo 17:1-8; Marko 9:2-8)**

37 [g][h]Kesho yake waliposhuka kutoka
mlimani, alikutana na umati mkubwa wa
watu. 38 Mtu mmoja katika ule umati wa
watu akapaza sauti, akasema, “Mwalimu,
naomba umwangalie mwanangu, kwani
ndiye mtoto wangu wa pekee. 39 Mara kwa
mara pepo mchafu humpagaa na kumfanya
apige kelele, kisha humwangusha na kumtia
kifafa hata akatokwa na povu kinywani.
Huyo pepo mchafu anamtesa sana, na
hamwachi ila mara chache. 40 Niliwaomba
wanafunzi wako wamtoe huyo pepo
mchafu, lakini hawakuweza.”

41 [i]Yesu akawajibu, “Enyi kizazi
kisichoamini na kilichopotoka! Nitakaa
nanyi na kuwavumilia mpaka lini? Mlete
mwanao hapa.”

42 [j]Hata yule mtoto alipokuwa akija, yule
pepo mchafu akamwangusha, akamtia
kifafa. Lakini Yesu akamkemea yule pepo
mchafu amtoke, akamponya yule mtoto, na
akamrudisha kwa baba yake. 43 Watu wote
wakastaajabia uweza mkuu wa Mungu.

Wakati bado watu walikuwa
wanastaajabia hayo yote aliyokuwa
akiyafanya Yesu, yeye akawaambia
wanafunzi wake: 44 [k]“Sikilizeni kwa makini
haya nitakayowaambia sasa: Mwana wa
Adamu atasalitiwa na kutiwa mikononi
mwa watu.” 45 [l]Lakini wao hawakuelewa
alimaanisha nini. Maana ya maneno hayo
ilifichika kwao, hivyo hawakuyaelewa, nao
wakaogopa kumuuliza maana yake.

*Ni Nani Atakayekuwa Mkubwa Kuliko Wote*

**(Mathayo 18:1-5; Marko 9:33-37)**

46 [m]Kukazuka mabishano miongoni mwa
wanafunzi kuhusu ni nani miongoni
mwao atakayekuwa mkuu kuliko wote.
47 [n]Lakini Yesu akayatambua mawazo
yao, naye akamchukua mtoto mdogo,
akamsimamisha kando yake. 48 [o]Kisha
akawaambia, “Yeyote amkaribishaye mtoto
huyu mdogo kwa Jina langu, anikaribisha
mimi, na yeyote atakayenikaribisha mimi,

[a]**9:28** Mt 4:21; Lk 3:21
[b]**9:31** 2Pet 1:15
[c]**9:32** Mt 26:43
[d]**9:33** Lk 5:5
[e]**9:35** Isa 42:12; Mt 3:17
[f]**9:36** Mt 17:9
[g]**9:37** Mt 17:14; Mk 9:14, 17
[h]**9:37** Mt 17:14-23; Mk 9:14-32
[i]**9:41** Kum 32:5
[j]**9:42** Lk 7:15
[k]**9:44** Lk 9:22; Mt 17:22
[l]**9:45** Mk 9:32
[m]**9:46** Lk 22:24
[n]**9:47** Mt 9:4
[o]**9:48** Mt 10:40; Mk 9:35

atakuwa amemkaribisha yeye aliyenituma.
Kwa maana yeye aliye mdogo miongoni
mwenu, ndiye aliye mkuu kuliko wote.”
49 [a]Yohana akasema, “Bwana, tumemwona
mtu akitoa pepo wachafu kwa jina lako,
nasi tukamzuia, kwa sababu yeye si mmoja
wetu.”
50 [b]Yesu akasema, “Msimzuie, kwa
sababu yeyote ambaye si kinyume nanyi,
yu upande wenu.”

*Yesu Akataliwa Samaria*

51 [c]Wakati ulipokaribia wa yeye
kuchukuliwa mbinguni, alikaza uso
wake kwenda Yerusalemu. 52 [d]Akatuma
watu wamtangulie, nao wakaenda katika
kijiji kimoja cha Samaria kumwandalia
kila kitu; 53 [e]lakini watu wa kijiji kile
hawakumkaribisha kwa sababu alikuwa
anakwenda zake Yerusalemu. 54 [f]Wanafunzi
wake, yaani Yakobo na Yohana, walipoona
hayo, wakasema: “Bwana, unataka tuagize
moto kutoka mbinguni ili uwaangamize?”
55 Yesu akageuka na kuwakemea, 56 [g]nao
wakaenda kijiji kingine.

*Gharama Ya Kumfuata Yesu*

**(Mathayo 8:19-22)**

57 [h]Walipokuwa njiani wakienda, mtu
mmoja akamwambia Yesu, “Nitakufuata
kokote uendako.”
58 [i]Yesu akamjibu, “Mbweha wana
mapango, nao ndege wa angani wana viota,
lakini Mwana wa Adamu hana mahali pa
kulaza kichwa chake.”
59 [j]Yesu akamwambia mtu mwingine,
“Nifuate.”
Mtu huyo akamjibu, “Bwana, niruhusu
kwanza nikamzike baba yangu.”
60 [k]Yesu akamwambia, “Waache wafu
wawazike wafu wao, bali wewe nenda
ukautangaze Ufalme wa Mungu.”
61 [l]Mtu mwingine akamwambia, “Bwana,
nitakufuata lakini naomba kwanza
nikawaage jamaa yangu.”
62 Yesu akamwambia, “Mtu yeyote atiaye
mkono wake kulima, kisha akatazama
nyuma, hafai kwa Ufalme wa Mungu.”

*Yesu Awatuma Wale Sabini Na Wawili*

10 [m]Baada ya hayo, Bwana akawachagua
wengine sabini na wawili, akawatuma
wawili wawili katika kila mji na kila
sehemu aliyokusudia kwenda baadaye.
2 [n]Akawaambia, “Mavuno ni mengi, lakini
watendakazi ni wachache. Kwa hiyo
mwombeni Bwana wa mavuno, ili apeleke
watendakazi katika shamba lake la mavuno.
3 [o]Haya! nendeni. Ninawatuma kama
wana-kondoo katikati ya mbwa mwitu.
4 [p]Msichukue mkoba, wala mfuko, wala
viatu, na msimsalimu mtu yeyote njiani.
5 [q]“Mkiingia katika nyumba yoyote,
kwanza semeni, ‘Amani iwe kwenu.’
6 Kama kuna mtu wa amani humo, basi
amani yenu itakuwa juu yake. La sivyo,
itawarudia. 7 [r]Kaeni katika nyumba hiyo,
mkila na kunywa kile watakachowapa, kwa
sababu kila mtendakazi anastahili malipo
yake. Msihamehame kutoka nyumba hadi
nyumba.
8 [s]“Mkienda katika mji na watu wake
wakawakaribisha, kuleni chochote
kiwekwacho mbele yenu, 9 [t]waponyeni
wagonjwa waliomo na waambieni: ‘Ufalme
wa Mungu umekaribia.’ 10 Lakini mkiingia
katika mji, nao hawakuwakaribisha,
tokeni mwende katika barabara zake

---

[a]**9:49** Mk 9:38; Hes 11:28
[b]**9:50** Mt 12:30; Lk 11:23
[c]**9:51** Mk 16:19; Lk 18:31; 19:28
[d]**9:52** Mt 10:5
[e]**9:53** Yn 4:9; 4:4
[f]**9:54** Mt 4:21; 2Fal 10:12
[g]**9:56** Yn 3:17; 12:27
[h]**9:57** Mt 8:19
[i]**9:58** Mt 8:20
[j]**9:59** Mt 4:19
[k]**9:60** Mt 3:2
[l]**9:61** 1Fal 19:20
[m]**10:1** Lk 7:13; 9:1-2, 51-52; Mk 6:7; Mt 10:1
[n]**10:2** Mt 9:37-38; Yn 4:35
[o]**10:3** Mt 10:16
[p]**10:4** Lk 9:3-5; 2Fal 4:29
[q]**10:5** Mt 4:12
[r]**10:7** Mt 10:10; 1Kor 9:14
[s]**10:8** 1Kor 10:27
[t]**10:9** Mt 3:2; 10:7

mkaseme: 11 [a]‘Hata mavumbi ya mji
wenu yaliyoshikamana na miguu yetu,
tunayakung’uta dhidi yenu. Lakini mjue
kwamba Ufalme wa Mungu umekaribia.’
12 [b]Ninawaambia, itakuwa rahisi zaidi kwa
Sodoma kustahimili katika siku ile kuliko
mji ule.

*Onyo Kwa Miji Isiyotubu*

**(Mathayo 11:20-24)**

13 [c]“Ole wako Korazini! Ole wako
Bethsaida! Kwa kuwa kama miujiza
iliyofanyika kwenu ingefanyika Tiro na
Sidoni, miji hiyo ingekuwa imetubu zamani,
kwa kuvaa magunia na kujipaka majivu.
14 Lakini itakuwa rahisi zaidi kwa Tiro na
Sidoni kustahimili katika siku ya hukumu,
kuliko ninyi. 15 [d]Nawe, Kapernaumu, je,
utainuliwa hadi mbinguni? La hasha,
utashushwa mpaka kuzimu.”

16 [e]“Yeye awasikilizaye ninyi anisikiliza
mimi; naye awakataaye ninyi amenikataa
mimi. Lakini yeye anikataaye mimi amkataa
yeye aliyenituma.”

17 [f]Wale sabini na wawili wakarudi kwa
furaha, na kusema, “Bwana, hata pepo
wachafu wanatutii kwa jina lako.”

18 [g]Yesu akawaambia, “Nilimwona
Shetani akianguka kutoka mbinguni kama
umeme wa radi. 19 [h]Tazama nimewapa
mamlaka ya kukanyaga nyoka na nge na
juu ya nguvu zote za adui; wala hakuna
kitu chochote kitakachowadhuru. 20 [i]Basi,
msifurahi kwa kuwa pepo wachafu
wanawatii, bali furahini kwa kuwa majina
yenu yameandikwa mbinguni.”

*Yesu Anashangilia*

**(Mathayo 11:25-27; 13:16-17)**

21 [j]Wakati huo Yesu akashangilia katika
Roho Mtakatifu, akasema, “Nakuhimidi
Baba, Bwana wa mbingu na nchi, kwa kuwa
umewaficha mambo haya wenye hekima na
wenye elimu, nawe ukawafunulia watoto
wadogo. Naam, Baba, kwa kuwa hivyo
ndivyo ilivyokupendeza.

22 [k]“Nimekabidhiwa vitu vyote na Baba
yangu. Hakuna mtu amjuaye Mwana ni
nani ila Baba, wala hakuna amjuaye Baba ni
nani ila Mwana na yeyote ambaye Mwana
anapenda kumfunulia.”

23 [l]Basi Yesu akawageukia wanafunzi
wake akanena nao faraghani, akawaambia,
“Heri macho yanayoona yale mambo
mnayoyaona. 24 [m]Kwa maana nawaambia,
manabii wengi na wafalme walitamani
kuona yale mnayoyaona lakini
hawakuyaona, na walitamani kusikia yale
mnayoyasikia lakini hawakuyasikia.”

*Mfano Wa Msamaria Mwema*

25 [n]Wakati huo mtaalamu mmoja wa sheria
alisimama ili kumjaribu Yesu, akamuuliza,
“Mwalimu, nifanye nini ili niurithi uzima
wa milele?”

26 Yesu akamjibu, “Imeandikwaje katika
Sheria? Kwani unasoma nini humo?”

27 [o]Akajibu, “ ‘Mpende Bwana Mungu
wako kwa moyo wako wote, kwa roho yako
yote, kwa nguvu zako zote, na kwa akili
zako zote’; tena, ‘Mpende jirani yako kama
unavyojipenda mwenyewe.’ ”

28 [p]Yesu akamwambia, “Umejibu vyema.
Fanya hivyo nawe utaishi.”

29 [q]Lakini yule mtaalamu wa sheria,
akitaka kujionyesha kuwa mwenye haki,
akamuuliza Yesu, “Jirani yangu ni nani?”

30 Yesu akamjibu akasema, “Mtu mmoja
alikuwa akiteremka kutoka Yerusalemu

[a]**10:11** Mt 10:14; Mk 6:11
[b]**10:12** Mt 10:15; 11:24
[c]**10:13** Lk 6:24-26; Ufu 11:3
[d]**10:15** Mt 4:13; Mwa 11:4; Kum 1:28; Isa 14:13; Yer 51:53
[e]**10:16** Mt 10:40; Yn 13:20
[f]**10:17** Mk 16:17
[g]**10:18** Mt 4:10; Isa 14:12; Ufu 9:1
[h]**10:19** Mk 16:18; Mdo 28:3-5
[i]**10:20** Dan 12:1; Flp 4:3
[j]**10:21** 1Kor 1:26-29
[k]**10:22** Mt 28:18; Yn 1:18
[l]**10:23** Mt 13:16, 17
[m]**10:24** 1Pet 1:10-12
[n]**10:25** Mt 19:16; Lk 18:18
[o]**10:27** Kum 6:5; Law 19:18; Mt 5:43
[p]**10:28** Law 18; 5; Rum 7:10
[q]**10:29** Lk 16:15

kwenda Yeriko, naye akaangukia
mikononi mwa wanyang'anyi. Wakampiga,
wakaondoka, wakamwacha akiwa karibu
kufa. 31 [a]Kuhani mmoja alikuwa akipitia njia
ile, alipomwona huyo mtu, akapita upande
mwingine, akamwacha hapo barabarani.
32 Vivyo hivyo, Mlawi mmoja naye alipofika
mahali pale, alimwona, akapita upande
mwingine, akamwacha hapo barabarani
33 [b]Lakini Msamaria mmoja aliyekuwa
akisafiri alipomwona, alimhurumia.
34 Akaenda alipokuwa na akasafisha
majeraha yake kwa divai na mafuta, kisha
akayafunga. Ndipo akampandisha kwenye
punda wake, akampeleka mpaka kwenye
nyumba ya wageni na kumtunza. 35 Kesho
yake, yule Msamaria akachukua dinari
mbili[c] akampa yule mwenye nyumba ya
wageni na kusema, 'Mtunze, nami nirudipo
nitakulipa gharama yoyote ya ziada
uliyotumia kwa ajili yake.'

36 "Ni yupi basi miongoni mwa hawa
watatu wewe unadhani ni jirani yake
yule mtu aliyeangukia mikononi mwa
wanyang'anyi?"

37 Yule mtaalamu wa sheria akajibu, "Ni
yule aliyemhurumia."

Ndipo Yesu akamwambia, "Nenda,
ukafanye vivyo hivyo."

### *Yesu Awatembelea Martha Na Maria*

38 [d]Ikawa Yesu na wanafunzi wake
walipokuwa wakienda Yerusalemu,
akaingia kwenye kijiji kimoja ambapo
mwanamke mmoja aliyeitwa Martha
alimkaribisha nyumbani kwake. 39 [e]Martha
alikuwa na mdogo wake aliyeitwa Maria,
ambaye aliketi chini miguuni mwa Bwana
akisikiliza yale aliyokuwa akisema. 40 [f]Lakini
Martha alikuwa akihangaika na maandalizi
yote yaliyokuwa yafanyike. Martha akaja
kwa Yesu na kumuuliza, "Bwana, hujali
kwamba ndugu yangu ameniachia kazi zote
mwenyewe? Basi mwambie anisaidie."

41 [g]Lakini Bwana akamjibu, "Martha,
Martha, mbona unasumbuka na kuhangaika
na mengi? 42 [h]Lakini kunahitajika kitu kimoja
tu. Maria amechagua kile kilicho bora, wala
hakuna mtu atakayemwondolea."

### *Yesu Afundisha Wanafunzi Wake Kuomba*

**(Mathayo 6:9-13; 7:7-11)**

11 [i]Siku moja, Yesu alikuwa mahali fulani
akiomba. Alipomaliza kuomba, mmoja
wa wanafunzi wake akamwambia, "Bwana,
tufundishe kuomba, kama vile Yohana
alivyowafundisha wanafunzi wake."

2 [jk]Akawaambia, "Mnapoomba, semeni:

" 'Baba yetu (uliye mbinguni),
jina lako litukuzwe,
ufalme wako uje.
(Mapenzi yako yafanyike
hapa duniani kama huko
mbinguni.)
3 Utupatie kila siku riziki yetu.
4 [l]Utusamehe dhambi zetu,
kwa kuwa na sisi huwasamehe
wote wanaotukosea.
Wala usitutie majaribuni
(bali utuokoe kutoka kwa yule
mwovu).' "

5 Kisha akawaambia, "Ni nani
miongoni mwenu mwenye rafiki yake,
naye akamwendea usiku wa manane na
kumwambia, 'Rafiki, nikopeshe mikate
mitatu. 6 Kwa sababu rafiki yangu amekuja
kutoka safarini, nami sina kitu cha kumpa.'

7 [m]"Kisha yule aliyeko ndani amjibu,
'Usinisumbue. Mlango umefungwa, nami
na watoto wangu tumelala. Siwezi kuamka
nikupe chochote.' 8 [n]Nawaambia, ingawa
huyo mtu hataamka na kumpa hiyo mikate
kwa sababu ni rafiki yake, lakini kwa sababu

---

[a]**10:31** Law 21:1-3
[b]**10:33** Mt 10:5
[c]35 Dinari mbili ni sawa na mshahara wa kibarua wa siku mbili.
[d]**10:38** Yn 11:1; 12:2-3
[e]**10:39** Lk 8:35
[f]**10:40** Mk 4:38
[g]**10:41** Mt 6:25-34; Lk 12:11, 22
[h]**10:42** Za 27:4
[i]**11:1** Lk 3:21; Yn 13:13
[j]**11:2** Mt 3:2
[k]**11:2** Mt 6:9-13
[l]**11:4** Mt 18:35; Mk 11:25; Mt 26:41; Yak 1:13
[m]**11:7** Mt 26:10
[n]**11:8** Lk 18:1-6

ya kuendelea kwake kuomba, ataamka na
kumpa kiasi anachohitaji.
9 [ab]“Kwa hiyo nawaambia: Ombeni nanyi
mtapewa; tafuteni nanyi mtapata; bisheni
nanyi mtafunguliwa mlango. 10 Kwa kuwa
kila aombaye hupewa; naye kila atafutaye
hupata; na kila abishaye hufunguliwa
mlango.
11 “Je, kuna yeyote miongoni mwenu
ambaye mtoto wake akimwomba samaki,
atampa nyoka badala yake? 12 Au mtoto
akimwomba yai atampa nge? 13 Basi ikiwa
ninyi mlio waovu, mnajua kuwapa watoto
wenu vitu vizuri, si zaidi sana Baba yenu
aliye mbinguni atawapa Roho Mtakatifu
wale wamwombao!”

*Yesu Na Beelzebuli*

**(Mathayo 12:22-30; Marko 3:20-27)**

14 [cd]Basi Yesu alikuwa anamtoa pepo
mchafu kutoka kwa mtu aliyekuwa bubu.
Yule pepo mchafu alipomtoka yule mtu
aliyekuwa bubu, akaanza kuongea, nao
umati wa watu ukashangaa. 15 [e]Lakini
wengine wakasema, “Anatoa pepo wachafu
kwa uwezo wa Beelzebuli,[f] yule mkuu
wa pepo wachafu wote.” 16 [g]Wengine ili
kumjaribu wakataka awaonyeshe ishara
kutoka mbinguni.
17 [h]Yesu akajua mawazo yao, naye
akawaambia, “Kila ufalme ukigawanyika
dhidi yake wenyewe huangamia. Nayo
nyumba iliyogawanyika dhidi yake yenyewe
itaanguka. 18 [i]Kama Shetani amegawanyika
mwenyewe, ufalme wake utasimamaje?
Nawaambia haya kwa sababu ninyi mnadai
ya kuwa mimi ninatoa pepo wachafu kwa
uwezo wa Beelzebuli. 19 [j]Kama mimi natoa
pepo wachafu kwa nguvu za Beelzebuli,
wafuasi wenu nao je, wao hutoa pepo
wachafu kwa uwezo wa nani? Hivyo basi,
wao ndio watakaowahukumu. 20 [k]Lakini
kama mimi ninatoa pepo wachafu kwa
kidole cha Mungu, basi Ufalme wa Mungu
umewajia.
21 [l]“Mtu mwenye nguvu aliyejifunga
silaha anapoilinda nyumba yake, mali
yake iko salama. 22 [m]Lakini mtu mwenye
nguvu zaidi kumliko akimshambulia na
kumshinda, yeye humnyang’anya silaha
zake zote alizozitegemea, na kuchukua
nyara.
23 [n]“Mtu asiyekuwa pamoja nami yu
kinyume nami, na mtu ambaye hakusanyi
pamoja nami, hutawanya.

*Kurudi Kwa Pepo Mchafu*

**(Mathayo 12:43-45)**

24 [o]“Pepo mchafu amtokapo mtu,
hutangatanga katika sehemu zisizo na
maji akitafuta mahali pa kupumzika,
lakini hapati. Ndipo husema, ‘Nitarudi
kwenye nyumba yangu nilikotoka.’ 25 Naye
arudipo na kuikuta ile nyumba imefagiliwa
na kupangwa vizuri, 26 [p]ndipo huenda na
kuchukua pepo wachafu wengine saba
wabaya kuliko yeye mwenyewe, nao
huingia na kukaa humo. Nayo hali ya
mwisho ya yule mtu huwa ni mbaya kuliko
ile ya kwanza.”
27 [q]Ikawa Yesu alipokuwa akisema hayo,
mwanamke mmoja katikati ya ule umati wa
watu akapaza sauti akasema, “Limebarikiwa
tumbo lililokuzaa na matiti uliyonyonya!”
28 [r]Yesu akajibu, “Wamebarikiwa zaidi
wale wanaolisikia neno la Mungu na
kulitii.”

---

[a]**11:9** Mt 7:7
[b]**11:9** Mt 7:7-11
[c]**11:14** Mt 9:32-33
[d]**11:14** Mt 12:22
[e]**11:15** Mk 3:22; Mt 9:34
[f]15 Beelzebubu au Beelzebuli; ni mkuu wa pepo wachafu; pia 18, 19.
[g]**11:16** Mt 12:38
[h]**11:17** Mt 9:34
[i]**11:18** Mt 4:10
[j]**11:19** Mk 11:24; Yn 15:7; Yak 1:6; Yn 3:32; Mt 7:7
[k]**11:20** Kut 8:19; Mt 3:2
[l]**11:21** Mt 12:29; Mk 3:17
[m]**11:22** Isa 53:12; Kol 2:15
[n]**11:23** Mt 12:30; Mk 9:40
[o]**11:24** Mt 12:43
[p]**11:26** 2Pet 2:20
[q]**11:27** Lk 23:29
[r]**11:28** Ebr 4:12; Mit 8:32; Yn 14:21

*Ishara Ya Yona*

**(Mathayo 12:38-42)**

29 [a]Umati wa watu ulipokuwa unazidi
kuongezeka, Yesu akaendelea kusema,
“Hiki ni kizazi kiovu. Kinatafuta ishara,
lakini hakitapewa ishara yoyote isipokuwa
ile ya Yona. 30 [b]Kwa maana kama vile Yona
alivyokuwa ishara kwa watu wa Ninawi,
ndivyo Mwana wa Adamu atakavyokuwa
ishara kwa kizazi hiki. 31 [c]Malkia wa
Kusini atasimama wakati wa hukumu na
kuwahukumu watu wa kizazi hiki. Kwa
kuwa yeye alikuja kutoka miisho ya dunia
ili kuisikiliza hekima ya Solomoni. Na hapa
yupo aliye mkuu kuliko Solomoni. 32 [d]Siku
ya hukumu, watu wa Ninawi watasimama
pamoja na kizazi hiki na kukihukumu; kwa
maana wao walitubu waliposikia mahubiri
ya Yona. Na tazama, hapa yupo yeye aliye
mkuu kuliko Yona.

*Taa Ya Mwili*

**(Mathayo 5:15; 6:22-23)**

33 [e]“Hakuna mtu yeyote awashaye taa na
kuiweka mahali palipofichika au kuifunikia
chini ya bakuli. Badala yake huiweka juu
ya kinara chake, ili watu wote wanaoingia
waone nuru. 34 [fg]Jicho lako ni taa ya mwili
wako. Kama jicho lako ni zima, mwili
wako wote pia umejaa nuru. Lakini kama
jicho ni bovu, mwili wako wote pia umejaa
giza. 35 Kwa hiyo, hakikisha kwamba nuru
iliyoko ndani yako isiwe giza. 36 Basi ikiwa
mwili wako wote umejaa nuru, bila sehemu
yake yoyote kuwa gizani, basi utakuwa na
nuru kama vile taa ikuangazavyo kwa nuru
yake.”

*Yesu Awashutumu Mafarisayo Na Wanasheria*

**(Mathayo 23:1-36; Marko 12:38-40)**

37 [h]Yesu alipomaliza kuzungumza,
Farisayo mmoja alimwalika nyumbani
mwake kwa chakula. Yesu akaingia
na kuketi katika sehemu yake mezani.
38 [i]Yule Farisayo akashangaa kwamba Yesu
hakunawa kwanza kabla ya kula.

39 [j]Ndipo Bwana akamwambia, “Sasa,
enyi Mafarisayo, mnasafisha kikombe
na sahani kwa nje, lakini ndani mmejaa
unyang’anyi na uovu. 40 [k]Enyi wapumbavu!
Hamjui kuwa yeye aliyetengeneza nje ndiye
alitengeneza na ndani pia? 41 [l]Basi toeni
sadaka ya vile mlivyo navyo, na tazama,
vitu vyote vitakuwa safi kwenu.

42 [m]“Lakini ole wenu, Mafarisayo, kwa
maana mnampa Mungu zaka za mnanaa,
mchicha na kila aina ya mboga, lakini
mnapuuza haki na upendo wa Mungu.
Iliwapasa kufanya haya ya pili bila kupuuza
hayo ya kwanza.

43 [n]“Ole wenu Mafarisayo, kwa sababu
ninyi mnapenda kukalia viti vya mbele
katika masinagogi, na kusalimiwa kwa
heshima masokoni.

44 [o]“Ole wenu, kwa sababu ninyi ni kama
makaburi yasiyokuwa na alama, ambayo
watu huyakanyaga pasipo kujua.”

45 [p]Mtaalamu mmoja wa sheria akamjibu,
akasema, “Mwalimu, unaposema mambo
haya, unatutukana na sisi pia.”

46 [q]Yesu akamjibu, “Nanyi wataalamu wa
sheria, ole wenu, kwa sababu mnawatwika
watu mizigo mizito ambayo hawawezi
kubeba, wala ninyi wenyewe hamwinui
hata kidole kimoja kuwasaidia.

47 [r]“Ole wenu, kwa sababu ninyi
mnajenga makaburi ya manabii
waliouawa na baba zenu. 48 [s]Hivyo ninyi
mwashuhudia na mnathibitisha kile baba
zenu walichofanya. Wao waliwaua manabii,

[a]**11:29** Mt 12:38; Yn 1:17; Mt 16:4
[b]**11:30** Yn 1:17; 2:10
[c]**11:31** 1Fal 10:1; 2Nya 9:1
[d]**11:32** Yon 3:5
[e]**11:33** Mt 5:15; Mk 4:21
[f]**11:34** Mt 6:22; 27
[g]**11:34** Mt 6:22; 23
[h]**11:37** Lk 7:36; 14:1
[i]**11:38** Mk 7:3-4
[j]**11:39** Lk 7:13; Mt 23:25-26; Mk 7:20-23
[k]**11:40** Lk 12:20; 1Kor 15:36
[l]**11:41** Lk 12:33; Mdo 10:15
[m]**11:42** Lk 18:12; Kum 6:5; Mik 6:8; Mt 23:23
[n]**11:43** Mt 23:6-7; Mk 12:38-39
[o]**11:44** Mt 23:27-35
[p]**11:45** Mt 22:35
[q]**11:46** Mt 23:4
[r]**11:47** Mt 23:29
[s]**11:48** Mt 23:29-32; Mdo 7:51-53

nanyi mnawajengea makaburi. [49] [a]Kwa
sababu ya jambo hili, Mungu katika hekima
yake alisema, ‘Tazama, nitatuma kwao
manabii na mitume, nao watawaua baadhi
yao na wengine watawatesa.’ [50] Kwa hiyo
kizazi hiki kitawajibika kwa ajili ya damu
ya manabii iliyomwagwa tangu kuwekwa
misingi ya ulimwengu, [51] [b]tangu damu ya
Abeli mpaka damu ya Zekaria, aliyeuawa
kati ya madhabahu na mahali patakatifu.
Naam, nawaambia, kizazi hiki kitawajibika
kwa haya yote.
[52] [c]“Ole wenu ninyi wataalamu wa sheria,
kwa sababu mmeuondoa ufunguo wa
maarifa. Ninyi wenyewe hamkuingia, na
wale waliokuwa wanaingia mkawazuia.”
[53] Yesu alipoondoka huko, walimu wa
sheria na Mafarisayo wakaanza kumpinga
vikali na kumsonga kwa maswali,
[54] [d]wakivizia kumkamata kwa kitu
atakachosema ili wamshtaki.

*Maonyo Dhidi Ya Unafiki*

**(Mathayo 10:26-33)**

12 [e]Wakati huo, umati mkubwa wa watu
maelfu, walipokuwa wamekusanyika
hata wakawa wanakanyagana, Yesu
akaanza kuzungumza kwanza na wanafunzi
wake, akawaambia: “Jihadharini na
chachu ya Mafarisayo, yaani, unafiki
wao. [2] [fg]Hakuna jambo lolote lililositirika
ambalo halitafunuliwa, au lililofichwa
ambalo halitajulikana. [3] Kwa hiyo, lolote
mlilosema gizani litasikiwa nuruni. Na kile
mlichonong’ona masikioni mkiwa kwenye
vyumba vya ndani, kitatangazwa juu ya
paa.
[4] [h]“Nawaambieni rafiki zangu,
msiwaogope wale wauao mwili, lakini
baada ya hilo hawawezi kufanya lolote zaidi.
[5] [i]Lakini nitawaambia nani wa kumwogopa:
Mwogopeni yule ambaye baada ya kuua
mwili, ana mamlaka ya kuwatupa motoni.
Naam, nawaambia, mwogopeni huyo!
[6] Mnajua kwamba shomoro watano huuzwa
kwa senti mbili? Lakini Mungu hamsahau
hata mmoja wao. [7] [j]Naam, hata nywele za
vichwa vyenu zote zimehesabiwa. Hivyo
msiogope, kwa maana ninyi ni wa thamani
kubwa kuliko shomoro wengi.
[8] [k]“Ninawaambia kwamba yeyote
atakayenikiri mbele ya watu, Mwana wa
Adamu naye atamkiri mbele za malaika wa
Mungu. [9] [l]Lakini yeye atakayenikana mimi
mbele ya watu, Mwana wa Adamu naye
atamkana mbele ya malaika wa Mungu.
[10] [m]Naye kila atakayenena neno baya dhidi
ya Mwana wa Adamu atasamehewa, lakini
yeyote atakayemkufuru Roho Mtakatifu
hatasamehewa.
[11] [n]“Watakapowapeleka katika
masinagogi, na mbele ya watawala na
wenye mamlaka, msiwe na wasiwasi
kuhusu namna mtakavyojitetea au
mtakavyosema. [12] [o]Kwa maana Roho
Mtakatifu atawafundisha wakati huo huo
mnachopaswa kusema.”

*Mfano Wa Tajiri Mpumbavu*

[13] Mtu mmoja katika umati wa watu
akamwambia Yesu, “Mwalimu, mwambie
ndugu yangu tugawane naye urithi wetu.”
[14] [p]Lakini Yesu akamwambia, “Rafiki,
ni nani aliyeniweka mimi kuwa hakimu
wenu au msuluhishi juu yenu?” [15] [q]Ndipo
Yesu akawaambia, “Jihadharini! Jilindeni
na aina zote za choyo. Kwa maana maisha
ya mtu hayatokani na wingi wa mali alizo
nazo.”
[16] Kisha akawaambia mfano huu:
“Shamba la mtu mmoja tajiri lilizaa sana.
[17] Akawaza moyoni mwake, ‘Nifanye nini?
Sina mahali pa kuhifadhi mavuno yangu.’

---

[a]**11:49** 1Kor 1:24; Kol 2:3
[b]**11:51** Mwa 4:8; 2Nya 24:20-21; Mt 23:35-36
[c]**11:52** Mt 23:13
[d]**11:54** Mt 12:10; Mk 12:13
[e]**12:1** Mt 16:6-12; Mk 8:15
[f]**12:2** Mk 4:12; Lk 8:17
[g]**12:2** Mt 10:26-33
[h]**12:4** Yn 15:14-15
[i]**12:5** Ebr 10:31
[j]**12:7** Mt 10:30; 12:12
[k]**12:8** Lk 15:10
[l]**12:9** Mk 8:38; 2Tim 2:12
[m]**12:10** Mt 8:20; 12:31-32; Mk 3:28-29
[n]**12:11** Mt 10:17-19; Mk 13:11
[o]**12:12** Kut 4:12; Mt 10:20
[p]**12:14** Mdo 7:27
[q]**12:15** Ay 31:24; Za 62:10

18 “Ndipo huyo tajiri akasema, ‘Nitafanya
hivi: Nitabomoa ghala zangu za nafaka na
kujenga nyingine kubwa zaidi na huko
nitayahifadhi mavuno yangu yote na
vitu vyangu. 19 [a]Nami nitaiambia nafsi
yangu, “Nafsi, unavyo vitu vingi vizuri
ulivyojiwekea akiba kwa miaka mingi.
Pumzika; kula, unywe, ufurahi.” ’

20 [b]“Lakini Mungu akamwambia,
‘Mpumbavu wewe! Usiku huu uhai wako
unatakiwa. Sasa hivyo vitu ulivyojiwekea
akiba vitakuwa vya nani?’

21 [c]“Hivyo ndivyo ilivyo kwa wale
wanaojiwekea mali lakini hawajitajirishi
kwa Mungu.”

*Msiwe Na Wasiwasi*

**(Mathayo 6:25-34)**

22 [de]Kisha Yesu akawaambia wanafunzi
wake: “Kwa hiyo nawaambia, msisumbukie
maisha yenu kwamba mtakula nini; au
msumbukie miili yenu kwamba mtavaa
nini. 23 Maisha ni zaidi ya chakula, na mwili
ni zaidi ya mavazi. 24 [f]Fikirini ndege! Wao
hawapandi wala hawavuni, hawana ghala
wala popote pa kuhifadhi nafaka; lakini
Mungu huwalisha. Ninyi ni wa thamani
zaidi kuliko ndege! 25 Ni nani miongoni
mwenu ambaye kwa kujitaabisha kwake
anaweza kujiongezea hata saa moja zaidi
katika maisha yake? 26 Kama hamwezi
kufanya jambo dogo kama hilo, kwa nini
basi kuyasumbukia hayo mengine?

27 [g]“Angalieni maua jinsi yameavyo:
Hayafanyi kazi wala hayafumi. Lakini
nawaambia, hata Solomoni katika fahari
yake yote hakuvikwa vizuri kama mojawapo
ya hayo maua. 28 [h]Basi ikiwa Mungu
huyavika hivi majani ya shambani, ambayo
leo yapo, na kesho yanatupwa motoni, si
atawavika ninyi vizuri zaidi, enyi wa imani
haba! 29 Wala msisumbuke mioyoni mwenu
mtakula nini au mtakunywa nini. Msiwe na
wasiwasi juu ya haya. 30 [i]Watu wa mataifa
ya duniani husumbuka sana kuhusu vitu
hivi vyote, lakini Baba yenu anafahamu
kuwa mnahitaji haya yote. 31 [j]Bali utafuteni
Ufalme wa Mungu, na haya yote atawapa
pia.

*Utajiri Wa Mbinguni*

**(Mathayo 6:19-21)**

32 [k]“Msiogope enyi kundi dogo, kwa
maana Baba yenu ameona vyema kuwapa
ninyi Ufalme. 33 [l]Uzeni mali zenu mkawape
maskini. Jifanyieni mifuko isiyochakaa,
mkajiwekee hazina mbinguni isiyokwisha,
mahali ambapo mwizi hakaribii wala
nondo haharibu. 34 [m]Kwa sababu mahali
hazina yako ilipo, hapo ndipo moyo wako
utakapokuwa pia.

*Kukesha*

35 [n]“Kuweni tayari mkiwa mmevikwa
kwa ajili ya huduma na taa zenu
zikiwa zinawaka, 36 [o]kama watumishi
wanaomngojea bwana wao arudi kutoka
kwenye karamu ya arusi, ili ajapo na
kubisha mlango waweze kumfungulia
mara. 37 [p]Heri wale watumishi ambao
bwana wao atakapokuja atawakuta wakiwa
wanakesha. Amin, nawaambia, atajifunga
mkanda wake na kuwaketisha ili wale,
naye atakuja na kuwahudumia. 38 Itakuwa
heri kwa watumwa hao ikiwa bwana wao
atakapokuja atawakuta wamekesha hata
kama atakuja mnamo usiku wa manane,
au karibu na mapambazuko. 39 [q]Lakini
fahamuni jambo hili: Kama mwenye
nyumba angalijua saa mwizi atakuja,
asingaliiacha nyumba yake kuvunjwa.

[a]**12:19** Mhu 11:9; 1Kor 15:32; Yak 5:5
[b]**12:20** Yer 17:11; Lk 11:40; Ay 27:8; Za 39:6; 49:19
[c]**12:21** Mt 6:20; Lk 12:33; 1Tim 6:18, 19; Yak 2:5
[d]**12:22** Mt 6:25
[e]**12:22** Mt 6:25-33
[f]**12:24** Ay 38:41; Za 147:9
[g]**12:27** 1Fal 10:4-7
[h]**12:28** Mt 6:30
[i]**12:30** Lk 6:36; Mt 6:8
[j]**12:31** Mt 3:2; 19:29
[k]**12:32** Mt 14:27; 25:34
[l]**12:33** Mt 19:21; Mdo 2:45; Mt 6:20; Yak 5:2
[m]**12:34** Mt 6:21
[n]**12:35** Efe 6:14; 1Pet 1:13; Mt 25:1
[o]**12:36** Mt 25:1-13
[p]**12:37** Mt 24:42-46; 25:13; 20:28
[q]**12:39** 1The 5:2; 2Pet 3:10

40 [a]Ninyi nanyi hamna budi kuwa tayari,
kwa sababu Mwana wa Adamu atakuja saa
msiyotazamia.”

*Mtumishi Mwaminifu Na Yule Asiye Mwaminifu*

**(Mathayo 24:45-51)**

41 Ndipo Petro akamuuliza, “Bwana,
mfano huu unatuambia sisi peke yetu au
watu wote?”
42 [b]Yesu akamjibu, “Ni yupi basi wakili
mwaminifu na mwenye busara, ambaye
bwana wake atamfanya msimamizi juu ya
watumishi wake wote, ili awape watumishi
wengine chakula chao wakati unaofaa?
43 Heri mtumishi yule ambaye bwana wake
atakaporudi atamkuta akifanya hivyo.
44 [c]Amin nawaambia, atamweka mtumishi
huyo kuwa msimamizi wa mali yake yote.
45 [d]Lakini kama yule mtumishi atasema
moyoni mwake, ‘Bwana wangu anakawia
kurudi,’ kisha akaanza kuwapiga wale
watumishi wa kiume na wa kike, na kula
na kunywa na kulewa. 46 [e]Basi bwana wa
mtumishi huyo atakuja siku asiyodhani na
saa asiyoijua. Atamkata vipande vipande
na kumweka katika sehemu moja pamoja
na wale wasioamini.
47 [f]“Yule mtumishi anayefahamu vyema
mapenzi ya bwana wake na asijiandae wala
kufanya kama apendavyo bwana wake,
atapigwa kwa mapigo mengi. 48 [g]Lakini
yeyote ambaye hakujua naye akafanya
yale yastahiliyo kupigwa, atapigwa kidogo.
Yeyote aliyepewa vitu vingi, atadaiwa
vingi; na yeyote aliyekabidhiwa vingi,
kwake vitatakiwa vingi.

*Yesu Kuleta Mafarakano*

**(Mathayo 10:34-36)**

49 [h]“Nimekuja kuleta moto duniani;
laiti kama ungekuwa tayari umewashwa!
50 [i]Lakini ninao ubatizo ambao lazima
nibatizwe, nayo dhiki yangu ni kuu mpaka
ubatizo huo ukamilike! 51 [j]Mnadhani
nimekuja kuleta amani duniani? La,
nawaambia sivyo, nimekuja kuleta
mafarakano. 52 [k]Kuanzia sasa, kutakuwa na
watu watano katika nyumba moja, watatu
dhidi ya wawili, na wawili dhidi ya watatu.
53 [l]Watafarakana baba dhidi ya mwanawe
na mwana dhidi ya babaye, mama dhidi
ya bintiye na binti dhidi ya mamaye, naye
mama mkwe dhidi ya mkwewe na mkwe
dhidi ya mama mkwe wake.”

*Kutambua Majira*

**(Mathayo 16:2-3)**

54 [m]Pia Yesu akauambia ule umati wa watu,
“Mwonapo wingu likitokea magharibi,
mara mwasema, ‘Mvua itanyesha,’ nayo
hunyesha. 55 Nanyi mwonapo upepo wa
kusini ukivuma, ninyi husema, ‘Kutakuwa
na joto,’ na huwa hivyo. 56 [n]Enyi wanafiki!
Mnajua jinsi ya kutambua kuonekana kwa
dunia na anga. Inakuwaje basi kwamba
mnashindwa kutambua wakati huu wa
sasa?
57 “Kwa nini hamwamui wenyewe lililo
haki? 58 [o]Uwapo njiani na mshtaki wako
kwenda kwa hakimu, jitahidi kupatana
naye mkiwa njiani. La sivyo, atakupeleka
kwa hakimu, naye hakimu atakukabidhi
kwa afisa, naye afisa atakutupa gerezani.
59 [p]Nakuambia, hautatoka humo hadi uwe
umelipa senti ya mwisho.”

*Tubu, La Sivyo Utaangamia*

13 [q]Wakati huo huo, kulikuwa na
watu waliomwambia Yesu habari
za Wagalilaya ambao Pilato aliwaua,
na damu ya hao watu akaichanganya

[a]**12:40** Mk 13:33; Lk 21:36
[b]**12:42** Lk 7:13
[c]**12:44** Mt 24:47
[d]**12:45** Mt 24:48
[e]**12:46** Lk 12:40
[f]**12:47** Kum 25:2
[g]**12:48** Law 5:17; Hes 15:27-30
[h]**12:49** Lk 12:51
[i]**12:50** Mk 10:38; Yn 19:30
[j]**12:51** Mt 10:34; Lk 12:49; Mik 7:6; Yn 7:46; 9:16
[k]**12:52** Mt 10:35
[l]**12:53** Mik 7:6; Mt 10:21
[m]**12:54** Mt 16:2-3
[n]**12:56** Mt 16:3
[o]**12:58** Mt 5:25
[p]**12:59** Mt 5:26; Mk 12:42
[q]**13:1** Mt 27:2

na dhabihu yao waliyokuwa wanatoa.
2 [a]Yesu akawauliza, “Mnadhani kwamba
hawa Wagalilaya ambao walikufa kifo cha
namna hiyo walikuwa na dhambi kuwazidi
Wagalilaya wengine wote? 3 [b]La hasha!
Ninyi nanyi msipotubu, mtaangamia vivyo
hivyo. 4 [c]Au wale watu kumi na wanane
waliokufa walipoangukiwa na mnara huko
Siloamu: mnadhani wao walikuwa waovu
kuliko watu wote waliokuwa wanaishi
Yerusalemu? 5 [d]Nawaambia, la hasha! Ninyi
nanyi msipotubu, wote mtaangamia vivyo
hivyo.”

*Mfano Wa Mti Usiozaa Matunda*

6 [e]Kisha Yesu akawaambia mfano huu:
“Mtu mmoja alikuwa na mtini uliopandwa
katika shamba lake la mizabibu, akaja
ili kutafuta tini kwenye mti huo, lakini
hakupata hata moja. 7 [f]Hivyo akamwambia
mtunza shamba: ‘Tazama, kwa muda
wa miaka mitatu sasa nimekuwa nikija
kutafuta matunda kwenye mtini huu,
nami sikupata hata moja. Ukate! Kwa nini
uendelee kuharibu ardhi?’

8 [g]“Yule mtunza shamba akamjibu,
‘Bwana, uache tena kwa mwaka mmoja
zaidi, nami nitaupalilia na kuuwekea
mbolea. 9 Kama ukizaa matunda mwaka
ujao, vyema, la sivyo uukate.’ ”

*Yesu Amponya Mwanamke Kilema Siku Ya Sabato*

10 [h]Basi Yesu alikuwa akifundisha
katika sinagogi mojawapo siku ya Sabato.
11 [i]Wakati huo huo akaja mwanamke mmoja
aliyekuwa na pepo mchafu, naye alikuwa
amepinda mgongo kwa muda wa miaka
kumi na minane, wala alikuwa hawezi
kunyooka wima. 12 Yesu alipomwona,
akamwita, akamwambia, “Mwanamke,
uwe huru, umepona ugonjwa wako.”
13 [j]Yesu alipomwekea mikono yake, mara
akasimama wima akaanza kumtukuza
Mungu.

14 [k]Lakini kiongozi wa sinagogi
akakasirika kwa sababu Yesu alikuwa
ameponya mtu siku ya Sabato. Akaambia
ule umati wa watu, “Kuna siku sita ambazo
watu wanapaswa kufanya kazi. Katika siku
hizo, njooni mponywe, lakini si katika siku
ya Sabato.”

15 [l]Lakini Bwana akamjibu, “Enyi
wanafiki! Je, kila mmoja wenu hamfungulii
ng’ombe wake au punda wake kutoka zizini
akampeleka kumnywesha maji siku ya
Sabato? 16 [m]Je, huyu mwanamke, ambaye ni
binti wa Abrahamu, aliyeteswa na Shetani
akiwa amemfunga kwa miaka yote hii kumi
na minane, hakustahili kufunguliwa kutoka
kifungo hicho siku ya Sabato?”

17 [n]Aliposema haya, wapinzani wake
wakaaibika, lakini watu wakafurahi kwa
ajili ya mambo ya ajabu aliyoyafanya.

*Mfano Wa Punje Ya Haradali*

**(Mathayo 13:31-32; Marko 4:30-32)**

18 [o]Kisha Yesu akauliza, “Ufalme wa
Mungu unafanana na nini? Nitaufananisha
na nini? 19 [p]Umefanana na punje ya haradali
ambayo mtu aliichukua na kuipanda katika
shamba lake. Nayo ikakua, ikawa mti nao
ndege wa angani wakatengeneza viota vyao
kwenye matawi yake.”

*Mfano Wa Chachu*

**(Mathayo 13:33)**

20 Yesu akauliza tena, “Nitaufananisha
Ufalme wa Mungu na nini? 21 [q]Unafanana
na chachu ambayo mwanamke aliichukua
akaichanganya katika kiasi kikubwa cha
unga mpaka wote ukaumuka.”

[a]**13:2** Yn 9:2-3
[b]**13:3** Za 7:12
[c]**13:4** Yn 9:7-11
[d]**13:5** Mt 3:2; Mdo 2:38
[e]**13:6** Isa 5:2; Mt 21:19
[f]**13:7** Mt 3:10
[g]**13:8** 2Pet 3:9, 15
[h]**13:10** Mt 4:23
[i]**13:11** Lk 13:16
[j]**13:13** Mt 5:23
[k]**13:14** Mt 12:2; Lk 14:3; Kut 20:9; Mk 5:22
[l]**13:15** Lk 14:5
[m]**13:16** Lk 3:8; 19:9; Mt 4:10
[n]**13:17** Isa 66:5
[o]**13:18** Mt 3:2; 13:24
[p]**13:19** Lk 17:6; Mt 13:32
[q]**13:21** 1Kor 5:6

*Mlango Mwembamba*

**(Mathayo 7:13-14, 21-23)**

22 [a]Yesu akapita katika miji na vijiji,
akifundisha wakati alisafiri kwenda
Yerusalemu. 23 Mtu mmoja akamuuliza,
“Bwana, ni watu wachache tu
watakaookolewa?”

24 [b]Yesu akawaambia, “Jitahidini sana
kuingia kupitia mlango mwembamba,
kwa maana nawaambia wengi watajaribu
kuingia, lakini hawataweza. 25 [c]Wakati
mwenye nyumba atakapoondoka na
kufunga mlango, mtasimama nje mkibisha
mlango na kusema, ‘Bwana! Tufungulie
mlango!’

“Lakini yeye atawajibu, ‘Siwajui ninyi,
wala mtokako.’

26 [d]“Ndipo mtamjibu, ‘Tulikula na kunywa
pamoja nawe, tena ulifundisha katika mitaa
yetu.’

27 [e]“Lakini yeye atawajibu, ‘Siwajui ninyi,
wala mtokako. Ondokeni kwangu, ninyi
watenda maovu!’

28 [f]“Ndipo kutakuwako kilio na kusaga
meno, mtakapowaona Abrahamu, Isaki,
Yakobo na manabii wote wakiwa katika
Ufalme wa Mungu, lakini ninyi mkiwa
mmetupwa nje. 29 [g]Watu watatoka
mashariki na magharibi, kaskazini na
kusini, nao wataketi kwenye sehemu
walizoandaliwa karamuni katika Ufalme wa
Mungu. 30 [h]Tazama, kunao walio wa mwisho
watakaokuwa wa kwanza, nao wa kwanza
watakaokuwa wa mwisho.”

*Yesu Aomboleza Kwa Ajili Ya Yerusalemu*

**(Mathayo 23:37-39)**

31 [i]Wakati huo huo baadhi ya Mafarisayo
wakamwendea Yesu na kumwambia,
“Ondoka hapa uende mahali pengine kwa
maana Herode anataka kukuua.”

32 [j]Yesu akawajibu, “Nendeni
mkamwambie yule mbweha, ‘Ninafukuza
pepo wachafu na kuponya wagonjwa leo
na kesho, nami siku ya tatu nitaikamilisha
kazi yangu.’ 33 [k]Sina budi kuendelea na
safari yangu leo, kesho na kesho kutwa:
kwa maana haiwezekani nabii kufa mahali
pengine isipokuwa Yerusalemu.

34 [l]“Ee Yerusalemu, Yerusalemu,
uwauaye manabii na kuwapiga mawe wale
waliotumwa kwako! Mara ngapi nimetamani
kuwakusanya watoto wako pamoja, kama
vile kuku akusanyavyo vifaranga wake
chini ya mabawa yake, lakini hukutaka!
35 [m]Tazama nyumba yenu imeachwa ukiwa.
Ninawaambia, hamtaniona tena mpaka
wakati ule mtakaposema, ‘Amebarikiwa
yeye ajaye kwa jina la Bwana.’ ”

*Yesu Nyumbani Mwa Farisayo*

14 [n]Ikawa siku moja Yesu alipokuwa
amekwenda kula chakula kwa mmoja
wa viongozi wa Mafarisayo siku ya Sabato,
watu walikuwa wakimchunguza kwa
bidii. 2 Papo hapo mbele yake palikuwa
na mtu mmoja mwenye ugonjwa wa
kuvimba mwili. 3 [o]Yesu akawauliza wale
Mafarisayo na walimu wa sheria, “Je, ni
halali kuponya watu siku ya Sabato au la?”
4 Wakakaa kimya. Hivyo Yesu akamshika
yule mgonjwa mkono na kumponya,
akamruhusu aende zake.

5 [p]Kisha akawauliza, “Kama mmoja wenu
angekuwa na mtoto au ng’ombe wake
aliyetumbukia katika kisima siku ya Sabato,
je, hamtamvuta mara moja na kumtoa?”
6 Nao hawakuwa na la kusema.

*Unyenyekevu Na Ukarimu*

7 [q]Alipoona jinsi wageni walivyokuwa

[a]**13:22** Lk 9:51
[b]**13:24** Mt 7:13
[c]**13:25** Mt 7:23; 25:10-12
[d]**13:26** Mt 7:22, 23
[e]**13:27** Mt 25:41
[f]**13:28** Mt 8:11-12
[g]**13:29** Mal 1:11; Isa 49:12; 59:19; Za 107:3; Lk 14:15
[h]**13:30** Mt 19:30
[i]**13:31** Mt 14:1
[j]**13:32** Ebr 2:10
[k]**13:33** Mt 21:11
[l]**13:34** Mt 23:37
[m]**13:35** Yer 12:17; 25:2; Za 118:26; Mt 21:9
[n]**14:1** Lk 7:36; 11:37; Mt 12:10
[o]**14:3** Mt 22:25; 12:10
[p]**14:5** Lk 13:15
[q]**14:7** Lk 11:43

wanachagua mahali pa heshima wakati
wa kula, akawaambia mfano huu: 8 [a]“Mtu
akikualika arusini, usikae mahali pa mgeni
wa heshima kwa kuwa inawezekana
amealikwa mtu mheshimiwa kuliko wewe.
9 Kama mkifanya hivyo yule aliyewaalika
ninyi wawili atakuja na kukuambia,
‘Mpishe huyu mtu kiti chako.’ Ndipo kwa
aibu utalazimika kukaa katika nafasi ya
chini kabisa. 10 [b]Badala yake, unapoalikwa,
chagua nafasi ya chini, ili yule mwenyeji
wako atakapokuona atakuja na kukuambia,
‘Rafiki yangu, nenda kwenye nafasi iliyo
bora zaidi.’ Kwa jinsi hii utakuwa umepewa
heshima mbele ya wageni wenzako wote.
11 [c]Kwa maana kila mtu ajikwezaye
atashushwa, naye ajishushaye atakwezwa.”
12 Kisha Yesu akamwambia yule
aliyewaalika, “Uandaapo karamu ya
chakula cha mchana au cha jioni, usialike
rafiki zako au ndugu zako au jamaa zako au
majirani zako walio matajiri tu. Ukifanya
hivyo, wao nao wanaweza kukualika kwao,
nawe ukawa umelipwa kile ulichofanya na
kupata thawabu yako. 13 [d]Bali ufanyapo
karamu, waalike maskini, vilema na
vipofu, 14 [e]nawe utabarikiwa kwa sababu
hawa hawana uwezo wa kukulipa. Mungu
atakulipa wakati wa ufufuo wa wenye
haki.”

### *Mfano Wa Karamu Kuu*

**(Mathayo 22:1-10)**

15 [f]Mmoja wa wale waliokuwa pamoja
naye mezani aliposikia hivi akamwambia
Yesu, “Amebarikiwa mtu yule atakayekula
katika karamu ya Ufalme wa Mungu!”
16 [g]Yesu akamjibu, “Mtu mmoja alikuwa
anaandaa karamu kubwa, akaalika watu
wengi. 17 [h]Wakati wa karamu ulipofika,
akamtuma mtumishi wake akawaambie
wale walioalikwa, ‘Karibuni, kila kitu ki
tayari sasa.’
18 “Lakini wote, kila mmoja, wakaanza
kutoa udhuru: Wa kwanza akasema,
‘Nimenunua shamba, lazima niende
kuliona. Tafadhali niwie radhi.’
19 “Mwingine akasema, ‘Ndipo tu
nimenunua jozi tano za ng’ombe wa
kulimia, nami ninakwenda kuwajaribu,
tafadhali niwie radhi.’ 20 [i]Naye mwingine
akasema, ‘Nimeoa mke, kwa hiyo siwezi
kuja.’
21 [j]“Yule mtumishi akarudi, akampa
bwana wake taarifa. Ndipo yule mwenye
nyumba akakasirika, akamwagiza yule
mtumishi wake, akisema, ‘Nenda upesi
kwenye mitaa na vichochoro vya mjini
uwalete maskini, vilema, vipofu na viwete.’
22 “Yule mtumishi akamwambia, ‘Bwana,
yale uliyoniagiza nimefanya, lakini bado
ipo nafasi.’
23 “Ndipo yule bwana akamwambia
mtumishi wake, ‘Nenda kwenye barabara na
vijia vilivyoko nje ya mji na uwalazimishe
watu waingie ili nyumba yangu ipate kujaa.
24 [k]Kwa maana nawaambia, hakuna hata
mmoja wa wale walioalikwa atakayeionja
karamu yangu.’ ”

### *Gharama Ya Kuwa Mwanafunzi*

**(Mathayo 10:37-38)**

25 Umati mkubwa wa watu ulikuwa
ukisafiri pamoja na Yesu, naye akageuka,
akawaambia, 26 [l]“Mtu yeyote anayekuja
kwangu hawezi kuwa mwanafunzi wangu
kama hatanipenda mimi zaidi ya baba
yake na mama yake, mke wake na watoto
wake, ndugu zake na dada zake, naam,
hata maisha yake mwenyewe. 27 [m]Yeyote
asiyeuchukua msalaba wake na kunifuata
hawezi kuwa mwanafunzi wangu.
28 [n]“Ni nani miongoni mwenu ambaye
kama anataka kujenga nyumba, hakai
kwanza chini na kufanya makisio ya

---

[a]**14:8** Mit 25:6
[b]**14:10** Mit 25:6, 7
[c]**14:11** Mt 23:12; Lk 18:14
[d]**14:13** Neh 8:10, 12; Kum 14:29
[e]**14:14** Mdo 24:15; Yn 5:29
[f]**14:15** Isa 25:6; Ufu 19:9; Mt 3:2
[g]**14:16** Mt 22:2
[h]**14:17** Mit 9:2, 3
[i]**14:20** 1Kor 7:33
[j]**14:21** Lk 14:13
[k]**14:24** Mt 21:43; Mdo 13:46
[l]**14:26** Mt 10:37; Yn 12:25
[m]**14:27** Mt 10:38; Lk 9:23
[n]**14:28** Mit 24:27

gharama aone kama ana fedha za kutosha
kukamilisha? 29 La sivyo, akiisha kuweka
msingi, naye akiwa hana uwezo wa
kuikamilisha, wote waionao wataanza
kumdhihaki, 30 wakisema, 'Mtu huyu alianza
kujenga lakini hakuweza kukamilisha.'
31 "Au ni mfalme gani atokaye kwenda
kupigana vita na mfalme mwingine, ambaye
hakai chini kwanza na kufikiri iwapo akiwa
na jeshi la watu 10,000 ataweza kupigana
na yule anayekuja na jeshi la watu 20,000?
32 Kama hawezi, basi wakati yule mwingine
akiwa bado yuko mbali, yeye hutuma
ujumbe wa watu na kuomba masharti ya
amani. 33 [a]Vivyo hivyo, yeyote miongoni
mwenu ambaye hawezi kuacha vyote alivyo
navyo, hawezi kuwa mwanafunzi wangu.

*Chumvi Isiyofaa*

**(Mathayo 5:13; Marko 9:50)**

34 [b]"Chumvi ni nzuri, lakini chumvi ikiwa
imepoteza ladha yake, itafanywaje ili iweze
kukolea tena? 35 [c]Haifai ardhi wala kwa
lundo la mbolea, bali hutupwa nje.
"Mwenye masikio ya kusikia, na asikie."

*Mfano Wa Kondoo Aliyepotea*

**(Mathayo 18:12-14)**

15 [d]Basi watoza ushuru na wenye dhambi
wote walikuwa wanakusanyika
ili wapate kumsikiliza Yesu. 2 [e]Lakini
Mafarisayo na walimu wa sheria
wakanung'unika wakisema, "Huyu mtu
anawakaribisha wenye dhambi na kula
nao."
3 [f]Ndipo Yesu akawaambia mfano
huu: 4 [g]"Ikiwa mmoja wenu ana kondoo
mia moja, naye akapoteza mmoja wao,
je, hawaachi wale tisini na tisa nyikani
na kwenda kumtafuta huyo aliyepotea
mpaka ampate? 5 Naye akishampata,
humbeba mabegani mwake kwa furaha 6 [h]na
kwenda nyumbani. Kisha huwaita rafiki
zake na majirani, na kuwaambia, 'Furahini
pamoja nami; nimempata kondoo wangu
aliyepotea.' 7 [i]Nawaambieni, vivyo hivyo
kutakuwa na furaha zaidi mbinguni kwa
sababu ya mwenye dhambi mmoja atubuye,
kuliko kwa wenye haki tisini na tisa ambao
hawana haja ya kutubu."

*Mfano Wa Sarafu Iliyopotea*

8 "Au ikiwa mwanamke ana sarafu
za fedha kumi, naye akapoteza moja,
je, hawashi taa na kufagia nyumba na
kuitafuta kwa bidii mpaka aipate? 9 [j]Naye
akiisha kuipata, huwaita rafiki zake na
majirani na kuwaambia, 'Furahini pamoja
nami; nimeipata ile sarafu yangu ya fedha
iliyopotea.' 10 [k]Vivyo hivyo, nawaambia,
kuna furaha mbele ya malaika wa Mungu
juu ya mwenye dhambi mmoja atubuye."

*Mfano Wa Mwana Mpotevu*

11 [l]Yesu akaendelea kusema: "Kulikuwa
na mtu mmoja aliyekuwa na wana
wawili. 12 [m]Yule mdogo akamwambia baba
yake, 'Baba, nipe urithi wangu.' Hivyo
akawagawia wanawe mali yake.
13 [n]"Baada ya muda mfupi, yule mdogo
akakusanya vitu vyote alivyokuwa navyo,
akaenda nchi ya mbali, na huko akaitapanya
mali yake kwa maisha ya anasa. 14 Baada
ya kutumia kila kitu alichokuwa nacho,
kukawa na njaa kali katika nchi ile yote,
naye akawa hana chochote. 15 [o]Kwa hiyo
akaenda akaajiriwa na mwenyeji mmoja
wa nchi ile ambaye alimpeleka shambani
kwake kulisha nguruwe. 16 [p]Akatamani
kujishibisha kwa maganda waliyokula
wale nguruwe, wala hakuna mtu aliyempa
chochote.
17 "Lakini alipozingatia moyoni
mwake, akasema, 'Ni watumishi wangapi

[a]**14:33** Flp 3:7-8
[b]**14:34** Mk 9:50
[c]**14:35** Mt 5:13; 11:15
[d]**15:1** Lk 5:29
[e]**15:2** Mt 9:11
[f]**15:3** Mt 13:3
[g]**15:4** Yer 31:10; Lk 19:10
[h]**15:6** Lk 15:9
[i]**15:7** Lk 15:10
[j]**15:9** Lk 15:6
[k]**15:10** Lk 15:7
[l]**15:11** Mt 21:28
[m]**15:12** Kum 2:17
[n]**15:13** Lk 16:1
[o]**15:15** Law 11:7
[p]**15:16** Mit 23:31

walioajiriwa na baba yangu ambao wana
chakula cha kuwatosha na kusaza, bali
mimi hapa nakufa kwa njaa! 18 [a]Nitaondoka
na kurudi kwa baba yangu na kumwambia:
Baba, nimetenda dhambi mbele za
Mungu na mbele yako. 19 Sistahili tena
kuitwa mwanao; nifanye kama mmoja
wa watumishi wako.' 20 [b]Basi akaondoka,
akaenda kwa baba yake.

"Lakini alipokuwa bado yuko mbali,
baba yake akamwona, moyo wake ukajawa
na huruma. Akamkimbilia mwanawe,
akamkumbatia na kumbusu.

21 [c]"Yule mwana akamwambia baba yake,
'Baba, nimekosa mbele za Mungu na mbele
yako. Sistahili kuitwa mwanao tena.'

22 [d]"Lakini baba yake akawaambia
watumishi, 'Leteni upesi joho lililo bora
sana, tieni pete kidoleni mwake na viatu
miguuni mwake. 23 Leteni ndama aliyenona,
mkamchinje ili tuwe na karamu, tule na
kufurahi. 24 [e]Kwa maana huyu mwanangu
alikuwa amekufa na sasa yu hai tena;
alikuwa amepotea na sasa amepatikana!'
Nao wakaanza kufanya tafrija.

25 "Wakati huo, yule mwana mkubwa
alikuwa shambani. Alipokaribia nyumbani,
akasikia sauti ya nyimbo na watu wakicheza.
26 Akamwita mmoja wa watumishi na
kumuuliza, 'Kuna nini?' 27 Akamwambia,
'Ndugu yako amekuja, naye baba yako
amemchinjia ndama aliyenona kwa sababu
mwanawe amerudi nyumbani akiwa salama
na mzima.'

28 [f]"Yule mwana mkubwa akakasirika,
akakataa kuingia ndani. Basi baba yake
akatoka nje na kumsihi. 29 Lakini yeye
akamjibu baba yake, 'Tazama! Miaka
yote hii nimekutumikia na hata siku moja
sijaacha kutii amri zako, lakini hujanipa
hata mwana-mbuzi ili nifurahi na rafiki
zangu. 30 [g]Lakini huyu mwanao ambaye
ametapanya mali yako kwa makahaba
aliporudi nyumbani, wewe umemchinjia
ndama aliyenona!'

31 [h]"Baba yake akamjibu, 'Mwanangu,
umekuwa nami siku zote na vyote nilivyo
navyo ni vyako. 32 [i]Lakini ilitubidi tufurahi
na kushangilia kwa sababu huyu ndugu
yako alikuwa amekufa na sasa yu hai;
alikuwa amepotea naye amepatikana.' "

### *Mfano Wa Msimamizi Mjanja*

16 [j]Yesu akawaambia wanafunzi wake,
"Palikuwa na tajiri mmoja na
msimamizi wake. Ilisemekana kwamba
huyo msimamizi alikuwa anatumia vibaya
mali ya tajiri yake. 2 Hivyo huyo tajiri
akamwita na kumuuliza, 'Ni mambo gani
haya ninayoyasikia kukuhusu? Toa taarifa
ya usimamizi wako, kwa sababu huwezi
kuendelea kuwa msimamizi.'

3 "Yule msimamizi akawaza moyoni
mwake, 'Nitafanya nini sasa? Bwana wangu
ananiondoa katika kazi yangu. Sina nguvu
za kulima, nami ninaona aibu kuombaomba.
4 Najua nitakalofanya ili nikiachishwa kazi
yangu hapa, watu wanikaribishe nyumbani
kwao.'

5 "Kwa hiyo akawaita wadeni wote wa
bwana wake, mmoja mmoja. Akamuuliza
wa kwanza, 'Deni lako kwa bwana wangu
ni kiasi gani?'

6 "Akajibu, 'Galoni 800[k] za mafuta ya
mizeituni.'

"Msimamizi akamwambia, 'Chukua hati
ya deni lako, ibadilishe upesi, uandike
galoni 400.'

7 "Kisha akamuuliza wa pili, 'Wewe deni
lako ni kiasi gani?'

"Akajibu, 'Vipimo 1,000[l] vya ngano.'

"Yule msimamizi akamwambia, 'Chukua
hati yako, andika vipimo 800!'

8 [m]"Yule bwana akamsifu yule msimamizi
dhalimu kwa jinsi alivyotumia ujanja. Kwa
maana watu wa dunia hii wana ujanja
zaidi wanapojishughulisha na mambo ya

---

[a]**15:18** Law 26:40; Mt 3:2
[b]**15:20** Mwa 46:29; Mdo 20:37
[c]**15:21** Za 51:4
[d]**15:22** Zek 3:4; Ufu 6:11; Mwa 41:42
[e]**15:24** Efe 5:11; 1Tim 5:6
[f]**15:28** Yon 4:1
[g]**15:30** Lk 15:12-13; Mit 29:3
[h]**15:31** Yn 18:10
[i]**15:32** Mal 3:17
[j]**16:1** Lk 15:13, 30
[k]6 Galoni 800 ni sawa na lita 4,000.
[l]7 Vipimo 1,000 ni kama magunia 100.
[m]**16:8** Za 17:14; 18:26; Efe 5:8; 1The 5:5

dunia kuliko watu wa nuru. 9 [a]Nawaambia,
tumieni mali ya kidunia kujipatia marafiki,
ili itakapokwisha, mkaribishwe katika
makao ya milele.
10 [b]“Yeyote aliye mwaminifu katika
mambo madogo, pia ni mwaminifu hata
katika mambo makubwa, naye mtu ambaye
si mwaminifu katika mambo madogo pia
si mwaminifu katika mambo makubwa.
11 [c]Ikiwa hamkuwa waaminifu katika mali
ya kidunia, ni nani atakayewaaminia
mali ya kweli? 12 Nanyi kama hamkuwa
waaminifu na mali ya mtu mwingine, ni
nani atakayewapa iliyo yenu wenyewe?
13 [d]“Hakuna mtumishi awezaye
kuwatumikia mabwana wawili. Kwa
kuwa atamchukia huyu na kumpenda yule
mwingine, au atashikamana sana na huyu
na kumdharau yule mwingine. Hamwezi
kumtumikia Mungu pamoja na Mali.”[e]
14 [f]Mafarisayo, waliokuwa wapenda
fedha, waliyasikia hayo yote na wakamcheka
kwa dharau. 15 [g]Yesu akawaambia, “Ninyi
mnajionyesha kuwa wenye haki mbele za
wanadamu, lakini Mungu anaijua mioyo
yenu. Kwa maana vile vitu ambavyo
wanadamu wanavithamini sana, kwa
Mungu ni machukizo.

*Sheria Na Ufalme Wa Mungu*

16 [h]“Sheria na Manabii vilihubiriwa mpaka
kuja kwa Yohana Mbatizaji. Tangu wakati
huo habari njema za Ufalme wa Mungu
zinahubiriwa, na kila mmoja hujiingiza
kwa nguvu. 17 [i]Lakini ni rahisi zaidi mbingu
na dunia kupita kuliko hata herufi moja
kuondoka katika Sheria.
18 [j]“Mtu yeyote amwachaye mkewe na
kumwoa mwanamke mwingine anazini,
naye mwanaume amwoaye mwanamke
aliyetalikiwa anazini.

*Tajiri Na Lazaro*

19 [k]“Palikuwa na mtu mmoja tajiri
aliyevaa nguo za rangi ya zambarau na
kitani safi, ambaye aliishi kwa anasa kila
siku. 20 [l]Hapo penye mlango wake aliishi
maskini mmoja, jina lake Lazaro, mwenye
vidonda mwili mzima. 21 [m]Huyo Lazaro
alitamani kujishibisha kwa makombo
yaliyoanguka kutoka mezani kwa yule
tajiri. Hata mbwa walikuwa wakija na
kuramba vidonda vyake.
22 “Wakati ukafika yule maskini akafa,
nao malaika wakamchukua akae pamoja
na Abrahamu. Yule tajiri naye akafa na
akazikwa. 23 Kule kuzimu alipokuwa
akiteseka, alitazama juu, akamwona
Abrahamu kwa mbali, naye Lazaro alikuwa
karibu yake. 24 [n]Hivyo yule tajiri akamwita,
‘Baba Abrahamu, nihurumie na umtume
Lazaro achovye ncha ya kidole chake ndani
ya maji aupoze ulimi wangu, kwa sababu
nina maumivu makuu kwenye moto huu.’
25 [o]“Lakini Abrahamu akamjibu,
‘Mwanangu, kumbuka kwamba wakati wa
uhai wako ulipata mambo mazuri, lakini
Lazaro alipata mambo mabaya. Lakini
sasa anafarijiwa hapa na wewe uko katika
maumivu makuu. 26 Zaidi ya hayo, kati yetu
na ninyi huko kumewekwa shimo kubwa,
ili wale wanaotaka kutoka huku kuja huko
wasiweze, wala mtu yeyote asiweze kuvuka
kutoka huko kuja kwetu.’
27 “Akasema, ‘Basi, nakuomba, umtume
Lazaro aende nyumbani kwa baba yangu,
28 [p]maana ninao ndugu watano. Awaonye,
ili wasije nao wakafika mahali hapa pa
mateso.’
29 [q]“Abrahamu akamjibu, ‘Ndugu zako

---

[a]**16:9** Lk 11:13; Mt 19:21; Lk 12:33
[b]**16:10** Mt 25:21-23; Lk 19:17
[c]**16:11** Lk 16:9, 13
[d]**16:13** Mt 6:24
[e]13 Mali (au Utajiri) hapa inatoka neno Mamoni kwa Kiaramu au Mamona kwa Kiyunani.
[f]**16:14** 1Tim 3:3; Lk 23:35
[g]**16:15** Lk 10:29; 1Sam 16:7; Ufu 2:23
[h]**16:16** Mt 5:17; 11:12-13; 4:24
[i]**16:17** Mt 5:18
[j]**16:18** Rum 7:2-3; 1Kor 7:10-11
[k]**16:19** Eze 16:49
[l]**16:20** Mdo 3:2
[m]**16:21** Mt 15:27; Lk 5:22
[n]**16:24** Lk 3:8; Mt 5:22
[o]**16:25** Za 17:14; Lk 6:21-25
[p]**16:28** Mdo 20:23; 1The 4:6
[q]**16:29** Yn 1:45; Mdo 15:21; Lk 24:27, 44

wana Maandiko ya Mose na Manabii,
wawasikilize hao.’
30 [a]“Yule tajiri akasema, ‘Hapana, baba
Abrahamu, lakini mtu kutoka kwa wafu
akiwaendea, watatubu.’
31 “Abrahamu akamwambia, ‘Kama
wasipowasikiliza Mose na Manabii,
hawataweza kushawishika hata kama mtu
akifufuka kutoka kwa wafu.’ ”

*Yesu Afundisha Kuhusu Majaribu, Dhambi Na Imani*

**(Mathayo 18:6-7, 21-22; Marko 9:42)**

17 [b]Yesu akawaambia wanafunzi wake,
“Mambo yanayosababisha watu
watende dhambi hayana budi kutukia.
Lakini ole wake mtu yule anayeyasababisha.
2 [c]Ingekuwa heri kama mtu huyo
angefungiwa jiwe la kusagia shingoni na
kutoswa baharini, kuliko kumsababisha
mmojawapo wa hawa wadogo kutenda
dhambi. 3 [d]Kwa hiyo, jilindeni.
“Kama ndugu yako akikukosea mwonye,
naye akitubu, msamehe. 4 [e]Kama akikukosea
mara saba kwa siku moja na mara saba kwa
siku moja akaja kwako akisema, ‘Ninatubu,’
msamehe.”

*Imani*

5 [f]Mitume wake wakamwambia Bwana,
“Tuongezee imani.”
6 [g]Bwana akawajibu, “Kama mkiwa na
imani ndogo kama punje ya haradali,
mngeweza kuuambia mti huu wa mkuyu,
‘Ng’oka ukaote baharini,’ nao ungewatii.

*Wajibu Wa Mtumishi*

7 “Ikiwa mmoja wenu ana mtumishi
anayelima shambani au anayechunga
kondoo, je, mtumishi huyo arudipo
atamwambia, ‘Karibu hapa keti ule
chakula?’ 8 [h]Je, badala yake, hatamwambia,
‘Niandalie chakula, nile, jifunge unitumikie
ninapokula na kunywa; baadaye waweza
kula na kunywa?’ 9 Je, huyo mtu
atamshukuru mtumishi huyo kwa kutimiza
yale aliyoamriwa? 10 [i]Vivyo hivyo nanyi
mkiisha kufanya mliyoagizwa, semeni, ‘Sisi
tu watumishi tusiostahili; tumefanya tu yale
tuliyopaswa kufanya.’ ”

*Yesu Atakasa Wakoma Kumi*

11 [j]Yesu alipokuwa njiani akienda
Yerusalemu, alipitia mpakani mwa Samaria
na Galilaya. 12 [k]Alipokuwa akiingia kwenye
kijiji kimoja, watu kumi waliokuwa na
ukoma wakakutana naye. Wakasimama
mbali, 13 [l]wakapaza sauti, wakasema,
“Yesu, Bwana, tuhurumie!”
14 [m]Alipowaona akawaambia, “Nendeni
mkajionyeshe kwa makuhani.” Nao
walipokuwa njiani wakienda, wakatakasika.
15 [n]Mmoja wao alipoona kwamba
amepona, akarudi kwa Yesu, akimsifu
Mungu kwa sauti kuu. 16 [o]Akajitupa miguuni
mwa Yesu akamshukuru. Yeye alikuwa
Msamaria.
17 Yesu akauliza, “Je, hawakutakaswa
wote kumi? Wako wapi wale wengine
tisa? 18 Hakuna hata mmoja aliyeonekana
kurudi ili kumshukuru Mungu isipokuwa
huyu mgeni?” 19 [p]Yesu akamwambia, “Inuka
na uende zako, imani yako imekuponya.”

*Kuja Kwa Ufalme Wa Mungu*

**(Mathayo 24:23-28, 37-41)**

20 [q]Yesu alipoulizwa na Mafarisayo
Ufalme wa Mungu utakuja lini, yeye
akawajibu, “Ufalme wa Mungu hauji
kwa kuchunguza kwa bidii, 21 [r]wala watu

[a]**16:30** Lk 3:8
[b]**17:1** Mt 5:29; 18:7
[c]**17:2** Mk 10:24; Lk 10:21; Mt 5:29
[d]**17:3** Mt 18:15; Efe 4:32; Kol 3:13
[e]**17:4** Mt 18:21-22
[f]**17:5** Mk 6:30; Lk 7:13
[g]**17:6** Mt 13:31; 17:20; 21:21; Mk 9:23
[h]**17:8** Lk 12:37
[i]**17:10** 1Kor 9:16
[j]**17:11** Lk 9:51-52; Yn 4:3-4
[k]**17:12** Mt 8:2; Law 13:45-46
[l]**17:13** Lk 5:5
[m]**17:14** Law 14:2; Mt 8:4
[n]**17:15** Mt 9:8
[o]**17:16** Mt 10:5
[p]**17:19** Mt 9:22
[q]**17:20** Yn 18:36; 3:3
[r]**17:21** Mt 24:23; Yn 1:26; 12:35

hawatasema, 'Huu hapa,' au 'Ule kule,' kwa
maana Ufalme wa Mungu umo ndani yenu."
22 [a]Kisha Yesu akawaambia wanafunzi
wake, "Wakati utafika ambapo mtatamani
kuiona moja ya siku ya Mwana wa
Adamu, lakini hamtaiona. 23 [b]Watu
watawaambia, 'Yule kule!' Au, 'Huyu hapa!'
Msiwakimbilie. 24 [c]Kwa maana kama vile
umeme wa radi umulikavyo katika anga
kuanzia mwisho mmoja hadi mwingine,
ndivyo atakavyokuwa Mwana wa Adamu
katika siku yake. 25 [d]Lakini kwanza
itampasa kuteseka katika mambo mengi
na kukataliwa na kizazi hiki.
26 [e]"Kama ilivyokuwa siku za Noa, ndivyo
itakavyokuwa katika siku za Mwana wa
Adamu. 27 [f]Watu walikuwa wakila na
kunywa, wakioa na kuolewa, mpaka siku ile
Noa alipoingia katika safina. Ndipo gharika
ikaja na kuwaangamiza wote.
28 [g]"Ndivyo ilivyokuwa katika siku za
Loti: Watu walikuwa wakila na kunywa,
wakinunua na kuuza, wakilima na kujenga.
29 [h]Lakini siku ile Loti alipoondoka Sodoma,
ikanyesha mvua ya moto na kiberiti kutoka
mbinguni ukawaangamiza wote.
30 [i]"Hivyo ndivyo itakavyokuwa siku
ile Mwana wa Adamu atakapofunuliwa.
31 [j]Siku hiyo, mtu yeyote aliye juu ya dari ya
nyumba yake, hata vitu vyake vikiwa ndani
ya hiyo nyumba, asishuke kuvichukua.
Vivyo hivyo mtu aliye shambani
asirudi nyumbani kuchukua chochote.
32 [k]Mkumbukeni mke wa Loti! 33 [l]Mtu
yeyote anayejaribu kuyaokoa maisha yake
atayapoteza, na yeyote atakayeyapoteza
maisha yake atayaokoa. 34 [m]Nawaambia,
usiku huo watu wawili watakuwa wamelala
kitanda kimoja; naye mmoja atatwaliwa na
mwingine ataachwa. 35 [n]Wanawake wawili
watakuwa wanasaga nafaka pamoja; naye
mmoja atatwaliwa na mwingine ataachwa.
[ 36 Wanaume wawili watakuwa wanafanya
kazi pamoja shambani; mmoja atachukuliwa
na mwingine ataachwa.]"
37 [o]Kisha wakamuuliza, "Haya yatatukia
wapi Bwana?"
Akawaambia, "Pale ulipo mzoga, huko
ndiko tai watakapokusanyika."

*Mfano Wa Mjane Asiyekata Tamaa*

18 [p]Kisha Yesu akawapa wanafunzi
wake mfano ili kuwaonyesha kuwa
yawapasa kuomba pasipo kukata tamaa.
2 Akawaambia, "Katika mji mmoja
alikuwepo hakimu ambaye hakumwogopa
Mungu wala kumjali mtu. 3 [q]Katika mji huo
alikuwako mjane mmoja ambaye alikuwa
akija kwake mara kwa mara akimwomba,
'Tafadhali nipatie haki kati yangu na adui
yangu.'
4 "Kwa muda mrefu yule hakimu alikataa.
Lakini hatimaye akasema moyoni mwake,
'Ijapokuwa simwogopi Mungu wala simjali
mwanadamu, 5 [r]lakini kwa kuwa huyu
mjane ananisumbuasumbua, nitahakikisha
amepata haki yake ili asiendelee kunichosha
kwa kunijia mara kwa mara!' "
6 [s]Bwana akasema, "Sikilizeni asemavyo
huyu hakimu dhalimu. 7 [t]Je, Mungu
hatawatendea haki wateule wake
wanaomlilia usiku na mchana? Je, atakawia
kuwasaidia? 8 [u]Ninawaambia, atawapatia
haki upesi. Lakini je, Mwana wa Adamu
atakapokuja ataikuta imani duniani?"

*Mfano Wa Farisayo Na Mtoza Ushuru*

9 [v]Yesu akatoa mfano huu kwa wale
waliojiamini kuwa wao ni wenye haki na

[a]**17:22** Mt 8:20; 9:15; Lk 5:35
[b]**17:23** Mt 24:23; Mk 13:21
[c]**17:24** Mt 24:27
[d]**17:25** Mt 16:21; Lk 9:22; Mk 13:30; Lk 18:32
[e]**17:26** Mwa 6:5-8; 7:6-24
[f]**17:27** Mwa 7:7-23
[g]**17:28** Mwa 19:1-28
[h]**17:29** Mwa 19:1-28
[i]**17:30** 2Pet 3:4; Ufu 1:7
[j]**17:31** Mt 24:17-18; Mk 13:15-16
[k]**17:32** Mwa 19:26
[l]**17:33** Yn 12:25
[m]**17:34** Mt 24:40, 41; 1The 4:17
[n]**17:35** Mt 24:41
[o]**17:37** Mt 24:28
[p]**18:1** Rum 1:10; Kol 4:2
[q]**18:3** Isa 1:17
[r]**18:5** Lk 11:8
[s]**18:6** Lk 7:13
[t]**18:7** Za 88:1; Ufu 6:10
[u]**18:8** Mt 8:20; 16:27
[v]**18:9** Lk 16:15; Isa 65:5

kuwadharau wengine: 10 [a]"Watu wawili
walikwenda Hekaluni kusali, mmoja
wao alikuwa Farisayo na mwingine
alikuwa mtoza ushuru. 11 [b]Yule Farisayo,
akasimama, akasali hivi na kuomba kwake
mwenyewe: 'Mungu, nakushukuru kwa
sababu mimi si kama watu wengine ambao
ni wanyang'anyi, wadhalimu, na wazinzi,
wala kama huyu mtoza ushuru. 12 [c]Mimi
nafunga mara mbili kwa juma, na natoa
sehemu ya kumi ya mapato yangu.'
13 [d]"Lakini yule mtoza ushuru akasimama
mbali, wala hakuthubutu hata kuinua uso
wake kutazama mbinguni, bali alijipigapiga
kifuani na kusema: 'Mungu, nihurumie,
mimi mwenye dhambi.'
14 [e]"Nawaambia, huyu mtoza ushuru
alirudi nyumbani akiwa amehesabiwa haki
mbele za Mungu zaidi ya yule Farisayo.
Kwa maana yeyote ajikwezaye atashushwa,
na yeyote ajishushaye atakwezwa."

*Yesu Awabariki Watoto Wadogo*

**(Mathayo 19:13-15; Marko 10:13-16)**

15 [f]Pia, watu walikuwa wakimletea Yesu
watoto wachanga ili awaguse. Wanafunzi
wake walipoona hivyo, wakawakemea.
16 [g]Lakini Yesu akawaita wale watoto
waje kwake, akasema, "Waacheni watoto
wadogo waje kwangu, wala msiwazuie,
kwa maana Ufalme wa Mungu ni wa wale
walio kama hawa. 17 [h]Amin, nawaambia,
mtu yeyote asiyeupokea Ufalme wa Mungu
kama mtoto mdogo, hatauingia kamwe."

*Mtawala Tajiri*

**(Mathayo 19:16-30; Marko 10:17-31)**

18 [ij]Mtawala mmoja akamuuliza Yesu,
"Mwalimu mwema, nifanye nini ili niurithi
uzima wa milele?"
19 Yesu akamjibu, "Mbona unaniita
mwema? Hakuna yeyote aliye mwema
ila Mungu peke yake. 20 [k]Unazijua amri:
'Usizini, usiue, usiibe, usishuhudie uongo,
waheshimu baba yako na mama yako.' "
21 Akajibu, "Amri hizi zote nimezishika
tangu nikiwa mtoto."
22 [l]Yesu aliposikia haya, akamwambia,
"Bado kuna jambo moja ulilopungukiwa.
Nenda ukauze kila kitu ulicho nacho,
uwape maskini, nawe utakuwa na hazina
mbinguni. Kisha njoo, unifuate."
23 Aliposikia jambo hili, alisikitika sana
kwa maana alikuwa mtu mwenye mali
nyingi. 24 [m]Yesu akamtazama, akasema,
"Tazama jinsi ilivyo vigumu kwa tajiri
kuingia katika Ufalme wa Mungu! 25 Hakika
ni rahisi zaidi kwa ngamia kupita kwenye
tundu la sindano kuliko mtu tajiri kuingia
katika Ufalme wa Mungu."
26 Wale waliosikia haya wakauliza, "Ni
nani basi awezaye kuokoka?"
27 [n]Yesu akajibu, "Yasiyowezekana kwa
wanadamu yanawezekana kwa Mungu."
28 [o]Ndipo Petro akamjibu, "Tazama,
tumeacha vyote tulivyokuwa navyo
tukakufuata!"
29 [p]Yesu akajibu, "Amin, nawaambia,
hakuna hata mtu aliyeacha nyumba yake,
au mke, au ndugu, au wazazi au watoto
kwa ajili ya Ufalme wa Mungu 30 [q]ambaye
hatapewa mara nyingi zaidi ya hivyo katika
maisha haya, na hatimaye kupata uzima
wa milele ujao."

*Yesu Atabiri Kifo Chake Mara Ya Tatu*

**(Mathayo 20:17-19; Marko 10:32-34)**

31 [r]Yesu akawachukua wale wanafunzi
wake kumi na wawili kando na kuwaambia,

[a] **18:10** Mdo 3:1
[b] **18:11** Za 135:2; Isa 1; 15; 58:2; Ufu 3:17
[c] **18:12** Isa 58:3; Mt 9:14; Mal 3:8; Lk 11:42
[d] **18:13** Isa 66:2; Lk 23:48; 5:32; 1Tim 1:15
[e] **18:14** Mt 23:12; Lk 14:11
[f] **18:15** Mt 19:13; Lk 10:13
[g] **18:16** 1Kor 14:20; 1Pet 2:2
[h] **18:17** Mt 11:25; 18:3
[i] **18:18** Mt 19:16-29; Mk 10:17-30
[j] **18:18** Lk 10:25
[k] **18:20** Kut 20:12-16; Rum 13:9
[l] **18:22** Mdo 2:45; Mt 6:20
[m] **18:24** Mit 11:28
[n] **18:27** Mt 19:26
[o] **18:28** Mt 4:19
[p] **18:29** Kum 33:9
[q] **18:30** Mt 12:32; 25:46
[r] **18:31** Lk 9:51; Za 22; Mt 8:20

"Tunapanda kwenda Yerusalemu, na kila kitu kilichoandikwa na manabii kumhusu Mwana wa Adamu kitatimizwa. 32 [a]Kwa kuwa atatiwa mikononi mwa watu wasiomjua Mungu, nao watamdhihaki, watamtukana na kumtemea mate, watampiga mijeledi na kumuua. 33 [b]Naye siku ya tatu atafufuka."

34 [c]Wanafunzi wake hawakuelewa mambo haya, kwa kuwa maana yake ilikuwa imefichika kwao, nao hawakujua Yesu alikuwa anazungumzia nini.

*Yesu Amponya Kipofu Karibu Na Yeriko*

**(Mathayo 20:29-34; Marko 10:46-52)**

35 [de]Yesu alipokuwa anakaribia Yeriko, kipofu mmoja alikuwa ameketi kando ya njia akiomba msaada. 36 Kipofu huyo aliposikia umati wa watu ukipita, akauliza, "Kuna nini?" 37 [f]Wakamwambia, "Yesu wa Nazareti anapita."

38 [g]Akapaza sauti, akasema, "Yesu, Mwana wa Daudi, nihurumie!"

39 [h]Wale waliokuwa wametangulia mbele wakamkemea, wakamwambia akae kimya. Lakini yeye akapaza sauti zaidi, "Mwana wa Daudi, nihurumie!"

40 Yesu akasimama, akawaamuru wamlete huyo mtu kwake. Alipokaribia, Yesu akamuuliza, 41 "Unataka nikufanyie nini?"

Akajibu, "Bwana, nataka kuona."

42 [i]Yesu akamwambia, "Basi upate kuona. Imani yako imekuponya." 43 [j]Akapata kuona saa ile ile, akamfuata Yesu, huku akimsifu Mungu. Watu wote walipoona mambo hayo, nao wakamsifu Mungu.

[a]**18:32** Lk 23:1; Mt 16:21; Mdo 2:23
[b]**18:33** Mt 16:21
[c]**18:34** Mk 9:32; Lk 9:45
[d]**18:35** Lk 19:1-4
[e]**18:35** Mt 20:29-34; Mk 10:46-52
[f]**18:37** Mt 9:27; 17:15; Lk 18:13
[g]**18:38** Lk 18:39; Mt 9:27; 17:15; Lk 18:13
[h]**18:39** Lk 18:38
[i]**18:42** Mt 9:22
[j]**18:43** Mt 9:8; Lk 13:17

*Zakayo Mtoza Ushuru*

19 [k]Yesu akaingia Yeriko, naye alikuwa anapita katikati ya huo mji. 2 Tazama, palikuwa na mtu mmoja mkuu wa watoza ushuru naye alikuwa tajiri, jina lake Zakayo. 3 Yeye alikuwa akijitahidi kumwona Yesu ni mtu wa namna gani. Lakini kutokana na umati mkubwa wa watu hakuweza kwa sababu alikuwa mfupi wa kimo. 4 [l]Kwa hiyo akatangulia mbio mbele ya umati wa watu akapanda juu ya mkuyu ili amwone Yesu, kwa sababu angeipitia njia ile.

5 Yesu alipofika pale chini ya huo mkuyu, akatazama juu, akamwambia, "Zakayo, shuka upesi, kwa maana leo nitakuwa mgeni nyumbani kwako!" 6 Hivyo Zakayo akashuka upesi, akamkaribisha Yesu nyumbani kwake kwa furaha kubwa.

7 [m]Watu wote walipoona hivyo, wakaanza kunung'unika wakisema, "Amekwenda kuwa mgeni wa 'mtu mwenye dhambi.' "

8 [n]Lakini Zakayo akasimama na kumwambia Bwana, "Tazama, Bwana! Sasa hivi nusu ya mali yangu ninawapa maskini, nami kama nimemdhulumu mtu yeyote kitu chochote, nitamrudishia mara nne ya hicho kiwango."

9 [o]Ndipo Yesu akamwambia, "Leo, wokovu umeingia nyumbani humu, kwa sababu huyu naye ni mwana wa Abrahamu. 10 [p]Kwa maana Mwana wa Adamu amekuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea."

*Mfano Wa Fedha*

**(Mathayo 25:14-30)**

11 [q]Walipokuwa wanasikiliza haya, Yesu akaendelea kuwaambia mfano, kwa sababu alikuwa anakaribia Yerusalemu na watu walikuwa wakidhani ya kuwa Ufalme wa Mungu ulikuwa unakuja saa iyo hiyo. 12 [r]Hivyo akawaambia: "Mtu mmoja mwenye cheo kikubwa alisafiri kwenda

[k]**19:1** Lk 18:35
[l]**19:4** 1Fal 10:27; 1Nya 27:28; Lk 18:37
[m]**19:7** Mt 9:11
[n]**19:8** Lk 7:13; 3:12-13; Hes 5:7; Eze 33:14-15
[o]**19:9** Rum 4:16; Gal 3:17
[p]**19:10** Eze 34:12-16; Yn 3:17
[q]**19:11** Lk 17:20; Mt 3:2; Mdo 1:6
[r]**19:12** Mk 13:34; Mt 25:14

nchi ya mbali ili akapokee madaraka
ya kuwa mfalme, kisha arudi. 13 [a]Hivyo
akawaita kumi miongoni mwa watumishi
wake, na akawapa kila mmoja fungu la
fedha. Akawaambia, ‘Fanyeni biashara na
fedha hizi mpaka nitakaporudi.’

14 [b]“Lakini raiya wa nchi yake walimchukia
wakapeleka ujumbe na kusema, ‘Hatutaki
huyu mtu awe mfalme wetu.’

15 “Hata hivyo alirudi akiwa amekwisha
kupokea mamlaka ya ufalme, akawaita wale
watumishi wake aliokuwa amewaachia
fedha, ili afahamu ni faida kiasi gani
kila mmoja wao aliyopata kwa kufanya
biashara.

16 “Wa kwanza akaja na kusema, ‘Bwana,
kutokana na fedha uliyoniachia, nimepata
faida mara kumi zaidi.’

17 “Yule bwana akamjibu, ‘Umefanya
vizuri mtumishi mwema! Kwa sababu
umekuwa mwaminifu katika wajibu mdogo
sana, nakupa mamlaka juu ya miji kumi.’

18 “Wa pili naye akaja. Akasema, ‘Bwana,
fedha yako imeleta faida mara tano zaidi.’

19 “Bwana wake akajibu, ‘Nakupa
mamlaka juu ya miji mitano.’

20 “Kisha akaja yule mtumishi mwingine,
akasema, ‘Bwana, hii hapa fedha yako.
Niliitunza vizuri kwenye kitambaa.
21 [c]Nilikuogopa, kwa sababu wewe ni mtu
mgumu. Unachukua ambapo hukuweka
kitu, na unavuna mahali ambapo hukupanda
kitu.’

22 [d]“Bwana wake akamjibu,
‘Nitakuhukumu kwa maneno yako
mwenyewe, wewe mtumishi mwovu! Kama
ulifahamu kwamba mimi ni mtu mgumu,
nichukuaye mahali ambapo sikuweka kitu
na kuvuna mahali ambapo sikupanda,
23 kwa nini basi hukuweka fedha zangu
kwa watoa riba, ili nitakaporudi nichukue
iliyo yangu na riba yake?’

24 “Ndipo akawaambia wale waliokuwa
wamesimama karibu, ‘Mnyang’anyeni
fungu lake la fedha, mkampe yule mwenye
kumi.’

25 “Wakamwambia, ‘Bwana, mbona;
tayari anayo mafungu kumi!’

26 [e]“Akawajibu, ‘Nawaambia kwamba
kila aliye na kitu, ataongezewa. Lakini
yule asiye na kitu, hata alicho nacho
atanyang’anywa. 27 Lakini wale adui zangu
ambao hawakutaka mimi niwe mfalme
juu yao. Waleteni hapa mkawaue mbele
yangu.’ ”

### *Yesu Aingia Yerusalemu Kwa Ushindi*

**(Mathayo 21:1-11; Marko 11:1-11; Yohana 12:12-19)**

28 [f]Baada ya Yesu kusema haya,
alitangulia kupanda kwenda Yerusalemu.
29 [gh]Naye alipokaribia Bethfage na Bethania
kwenye mlima uitwao Mlima wa Mizeituni,
aliwatuma wanafunzi wake wawili,
akawaambia, 30 “Nendeni katika kijiji
kilichoko mbele yenu. Na mtakapokuwa
mnaingia kijijini, mtamkuta mwana-punda
amefungwa hapo, ambaye hajapandwa
na mtu bado. Mfungueni, mkamlete
hapa. 31 Kama mtu akiwauliza, ‘Mbona
mnamfungua?’ Mwambieni, ‘Bwana
anamhitaji.’ ”

32 [i]Wale waliotumwa wakaenda,
wakakuta kila kitu kama vile Yesu
alivyokuwa amewaambia. 33 [j]Walipokuwa
wanamfungua yule mwana-punda, wenyewe
wakawauliza, “Mbona mnamfungua huyo
mwana-punda?”

34 Wale wanafunzi wakajibu, “Bwana
anamhitaji.”

35 [k]Wakamleta kwa Yesu, nao baada ya
kutandika mavazi yao juu ya huyo mwana-
punda, wakampandisha Yesu juu yake.
36 [l]Alipokuwa akienda akiwa amempanda,
watu wakatandaza mavazi yao barabarani.

37 [m]Alipokaribia mahali yanapoanzia
materemko ya Mlima wa Mizeituni, umati

---

[a]**19:13** Mk 13:34
[b]**19:14** Yn 1:11
[c]**19:21** Mit 27:18; Lk 16:10
[d]**19:22** 2Sam 1:16; Ay 15:6; Mt 25:26
[e]**19:26** Mt 13:12; 25:29
[f]**19:28** Mk 10:32; Lk 9:51
[g]**19:29** Mt 21:1, 17
[h]**19:29** Mt 21:1-9; Mk 11:1-10; Yn 12:12-16
[i]**19:32** Lk 22:13
[j]**19:33** 2Fal 9:13
[k]**19:35** 2Fal 9:13; Mt 21:7; Mk 11:7; Yn 12:14
[l]**19:36** Mt 21:18
[m]**19:37** Mt 21:1

wote wa wafuasi wake wakaanza kumsifu
Mungu kwa furaha kwa sauti kuu kwa ajili
ya matendo yote ya miujiza waliyoyaona.
Wakasema:

38 [a]“Amebarikiwa Mfalme ajaye kwa
Jina la Bwana!”
“Amani mbinguni na utukufu huko
juu sana.”

39 [b]Baadhi ya Mafarisayo waliokuwamo
miongoni mwa ule umati wa watu
wakamwambia, “Mwalimu, waamuru
wanafunzi wako wanyamaze.”
40 [c]Yesu akawajibu, “Nawaambia ninyi,
kama hawa wakinyamaza, mawe yatapiga
kelele.”

*Yesu Anaulilia Mji Wa Yerusalemu*

41 [d]Alipokaribia Yerusalemu na kuuona
mji, aliulilia, 42 [e]akisema, “Laiti ungalijua
hata wewe leo yale ambayo yangeleta amani,
lakini sasa yamefichika machoni pako.
43 [f]Hakika siku zinakujia, ambazo adui zako
watakuzingira, nao watakuzunguka pande
zote na kukuzuilia ndani. 44 [g]Watakuponda
chini, wewe na watoto walioko ndani ya
kuta zako. Nao hawataacha hata jiwe moja
juu ya jingine, kwa sababu hukutambua
wakati wa kujiliwa kwako.”

*Yesu Atakasa Hekaluni*

**(Mathayo 21:12-17; Marko 11:15-19; Yohana 2:13-22)**

45 [h]Ndipo akaingia eneo la Hekalu,
akaanza kuwafukuza wale waliokuwa
wakiuza vitu humo. 46 [i]Naye akawaambia,
“Imeandikwa, ‘Nyumba yangu itakuwa
nyumba ya sala,’ lakini ninyi mmeifanya
kuwa ‘pango la wanyang’anyi.’ ”
47 [j]Kila siku alikuwa akifundisha
Hekaluni. Lakini viongozi wa makuhani,
walimu wa sheria na viongozi wa watu
walikuwa wakitafuta njia ili kumuua.
48 Lakini hawakupata nafasi kwa sababu
watu wote walimfuata wakiyasikiliza
maneno yake kwa usikivu mwingi.

*Swali Kuhusu Mamlaka Ya Yesu*

**(Mathayo 21:23-27; Marko 11:27-33)**

20 [k][l]Siku moja, Yesu alipokuwa
akifundisha watu Hekaluni na kuhubiri
habari njema, viongozi wa makuhani,
walimu wa sheria, pamoja na wazee wa
watu wakamjia. 2 [m]Wakamuuliza, “Tuambie,
unafanya mambo haya kwa mamlaka gani?
Ni nani aliyekupa mamlaka haya?”
3 Akawajibu, “Nami nitawauliza swali.
4 [n]Je, ubatizo wa Yohana ulitoka mbinguni
au kwa wanadamu?”
5 Wakahojiana wao kwa wao wakisema,
“Kama tukisema, ‘Ulitoka mbinguni,’
atatuuliza, ‘Mbona hamkumwamini?’
6 [o]Lakini tukisema, ‘Ulitoka kwa wanadamu,’
watu wote watatupiga mawe, kwa sababu
wanaamini kwamba Yohana alikuwa nabii.”
7 Basi wakajibu, “Hatujui ulikotoka.”
8 Yesu akawaambia, “Wala mimi
sitawaambia ni kwa mamlaka gani
ninatenda mambo haya.”

*Mfano Wa Wapangaji Waovu*

**(Mathayo 21:33-46; Marko 12:1-12)**

9 [p]Akaendelea kuwaambia watu mfano
huu: “Mtu mmoja alipanda shamba la
mizabibu, akalikodisha kwa wakulima
fulani, kisha akasafiri kwa muda mrefu.
10 [q]Wakati wa mavuno ulipofika, akamtuma
mtumishi wake kwa hao wapangaji ili
wampe sehemu ya mavuno ya shamba
la mizabibu. Lakini wale wakulima
wakampiga, wakamfukuza mikono mitupu.

[a]**19:38** Za 118:26; Lk 13:35; 2:14
[b]**19:39** Mt 21:15-16
[c]**19:40** Ebr 2:11
[d]**19:41** Isa 22:4; Lk 13:34-35
[e]**19:42** Kum 32:29; Mt 13:14; Yn 12:38
[f]**19:43** Yer 6:6; Lk 21:20
[g]**19:44** Za 137:9; Mt 24:2; Mk 13:2; 1Pet 2:12
[h]**19:45** Mt 21:12; Mk 11:11, 15; Yn 2:14, 15
[i]**19:46** Isa 56:7; Yer 7:11
[j]**19:47** Mt 26:55; 12:14; Mk 11:18
[k]**20:1** Mt 26:55; Lk 8:1
[l]**20:1** Mt 21:23-27; Mk 11:27-33
[m]**20:2** Yn 2:18; Mdo 4:7
[n]**20:4** Mk 1:4
[o]**20:6** Lk 7:29; Mt 11:9
[p]**20:9** Isa 5:17; Mt 25:14
[q]**20:10** 2Nya 36:15, 16

11 Akamtuma mtumishi mwingine, huyo
naye wakampiga, wakamfanyia mambo ya
aibu na kumfukuza. 12 Bado akamtuma na
mwingine wa tatu, huyu pia wakamjeruhi
na kumtupa nje ya shamba.
13 [a]“Basi yule mwenye shamba la
mizabibu akasema, ‘Nifanye nini?
Nitamtuma mwanangu mpendwa, huenda
yeye watamheshimu.’
14 “Lakini wale wapangaji walipomwona,
wakasemezana wao kwa wao. Wakasema,
‘Huyu ndiye mrithi. Basi na tumuue ili
urithi uwe wetu.’ 15 Kwa hiyo wakamtupa
nje ya shamba la mizabibu, wakamuua.”
“Sasa basi yule mwenye shamba la
mizabibu atawafanyia nini wapangaji hawa?
16 [b]Atakuja na kuwaua hao wapangaji, na
kuwapa wapangaji wengine hilo shamba
la mizabibu.”
Watu waliposikia hayo wakasema,
“Mungu apishie mbali jambo hili lisitokee!”
17 [c]Lakini Yesu akawakazia macho,
akasema, “Basi ni nini maana ya yale
yaliyoandikwa:

“ ‘Jiwe walilolikataa waashi,
limekuwa jiwe kuu la pembeni’?

18 [d]Kila mtu aangukaye juu ya jiwe hilo
atavunjika vipande vipande, lakini yule
litakayemwangukia atasagwa kabisa.”
19 [e]Walimu wa sheria na viongozi wa
makuhani wakatafuta njia ya kumkamata
mara moja, kwa sababu walifahamu
kwamba amesema mfano huo kwa ajili
yao. Lakini waliwaogopa watu.

*Kumlipa Kaisari Kodi*

**(Mathayo 22:15-22; Marko 12:13-17)**

20 [f]Kwa hiyo wakawa wanamchunguza
na kutuma wapelelezi waliojifanya kuwa
wenye haki ili wapate kumtega kwa
maneno asemayo, ili wamtie katika uwezo
na mamlaka ya mtawala. 21 [g]Hivyo wale
wapelelezi wakamuuliza, “Mwalimu,
tunajua unasema na kufundisha yaliyo kweli
wala humpendelei mtu, bali wafundisha
njia ya Mungu katika kweli. 22 Je, ni halali
sisi kulipa kodi kwa Kaisari, au la?”
23 Lakini Yesu akatambua hila yao, kwa
hiyo akawaambia, 24 “Nionyesheni dinari.
Je, sura hii na maandishi haya yaliyoko juu
yake ni vya nani?”
25 [h]Wakamjibu, “Ni vya Kaisari.”
Akawaambia, “Basi mpeni Kaisari kilicho
cha Kaisari, naye Mungu mpeni kilicho cha
Mungu.”
26 Wakashindwa kumkamata kwa yale
aliyokuwa amesema hadharani. Nao
wakashangazwa mno na majibu yake,
wakanyamaza kimya.

*Ufufuo Na Ndoa*

**(Mathayo 22:23-33; Marko 12:18-27)**

27 [i]Baadhi ya Masadukayo, wale wasemao
kwamba hakuna ufufuo wa wafu, wakamjia
Yesu na kumuuliza, 28 [j]“Mwalimu, Mose
alituandikia kwamba kama ndugu wa mtu
akifa na kumwacha mkewe bila mtoto,
basi huyo mtu inampasa amwoe huyo
mjane ili amzalie ndugu yake watoto.
29 Basi palikuwepo ndugu saba. Yule wa
kwanza akaoa, akafa bila kuzaa mtoto.
30 Kisha yule wa pili akamwoa huyo mjane,
naye akafa bila mtoto, 31 naye wa tatu pia
akamwoa. Vivyo hivyo ndugu wote saba
wakawa wamemwoa huyo mwanamke, na
wote wakafa pasipo yeyote kupata mtoto.
32 Mwishowe, yule mwanamke naye akafa.
33 Sasa basi, siku ya ufufuo huyo mwanamke
atakuwa mke wa nani, maana aliolewa na
ndugu wote saba?”
34 Yesu akawajibu, “Katika maisha haya
watu huoa na kuolewa. 35 [k]Lakini wale
ambao wamehesabiwa kwamba wanastahili
kupata nafasi katika ulimwengu ule na
katika ufufuo wa wafu, hawaoi wala

[a]**20:13** Mt 3:17
[b]**20:16** Lk 19:27
[c]**20:17** Za 118:22; Mdo 4:11
[d]**20:18** Isa 8:14-15
[e]**20:19** Lk 19:47; Mk 11:18
[f]**20:20** Mt 12:10; 27:2
[g]**20:21** Yn 3:2
[h]**20:25** Lk 23:2; Rum 13:7
[i]**20:27** Mdo 23:8; 1Kor 15:12; Mdo 4:1
[j]**20:28** Kum 25:5; Mwa 38:8
[k]**20:35** Mt 12:32

hawaolewi. 36 [a]Hawa hawawezi kufa tena,
kwa maana wao ni kama malaika. Wao ni
watoto wa Mungu, kwa sababu ni watoto
wa ufufuo. 37 [b]Hata Mose alidhihirisha
kuwa wafu wanafufuka, kwa habari ya kile
kichaka kilichokuwa kikiwaka moto bila
kuteketea, alipomwita Bwana, 'Mungu wa
Abrahamu, Mungu wa Isaki, na Mungu wa
Yakobo.' 38 [c]Yeye si Mungu wa wafu, bali wa
walio hai, kwa kuwa kwake wote ni hai."

39 Baadhi ya walimu wa sheria wakasema,
"Mwalimu, umesema sawasawa kabisa!"

40 [d]Baada ya hayo hakuna mtu
aliyethubutu kumuuliza maswali tena.

*Kristo Ni Mwana Wa Nani?*

**(Mathayo 22:41-46; Marko 12:35-37)**

41 [ef]Kisha Yesu akawaambia, "Imekuwaje
basi wao husema Kristo[g] ni Mwana wa
Daudi? 42 [h]Daudi mwenyewe anasema
katika Kitabu cha Zaburi:

" 'Bwana alimwambia Bwana wangu:
"Keti mkono wangu wa kuume,
43 [i]hadi nitakapowaweka adui zako
chini ya miguu yako." '

44 Ikiwa Daudi anamwita yeye 'Bwana,' basi
atakuwaje mwanawe?"

*Yesu Awashutumu Walimu Wa Sheria*

**(Mathayo 23:1-36; Marko 12:38-40)**

45 [j]Wakati watu wote walikuwa
wanamsikiliza, Yesu akawaambia
wanafunzi wake, 46 [k]"Jihadharini na walimu
wa sheria. Wao hupenda kutembea wakiwa
wamevaa mavazi marefu, na kusalimiwa
kwa heshima masokoni. Hupenda kukaa
kwenye viti vya mbele katika masinagogi,
na kukaa kwenye nafasi za heshima katika
karamu. 47 [l]Wao hula nyumba za wajane, na
ili waonekane kuwa wema, wanasali sala
ndefu. Watu kama hawa watapata hukumu
iliyo kuu sana."

*Sadaka Ya Mjane*

**(Marko 12:41-44)**

21 [m]Yesu alipoinua macho yake, aliwaona
matajiri wakiweka sadaka zao kwenye
sanduku la hazina ya Hekalu. 2 Akamwona
pia mjane mmoja maskini akiweka humo
sarafu mbili ndogo za shaba. 3 [n]Yesu
akasema, "Amin, nawaambia, huyu mjane
maskini ameweka humo zaidi ya watu
wengine wote. 4 [o]Hawa watu wengine wote
wametoa sadaka kutokana na wingi wa mali
zao. Lakini huyu mjane ametoa kutokana
na umaskini wake vyote alivyokuwa navyo,
hata kile alichohitaji ili kuishi."

*Dalili Za Siku Za Mwisho*

**(Mathayo 24:1-2; Marko 13:1-2)**

5 Baadhi ya wanafunzi wake
wakawa wanamwonyesha jinsi Hekalu
lilivyopambwa kwa mawe mazuri na kwa
vitu vilivyotolewa kuwa sadaka kwa Mungu.
Lakini Yesu akawaambia, 6 [p]"Kuhusu haya
mnayoyaona hapa, wakati utafika ambapo
hakuna jiwe moja litakalobaki juu ya
jingine, bali kila moja litabomolewa."

*Mateso*

**(Mathayo 24:3-14; Marko 13:3-13)**

7 Wakamuuliza, "Mwalimu, mambo haya
yatatukia lini? Ni dalili gani itaonyesha
kwamba yanakaribia kutendeka?"

8 [q]Yesu akawajibu, "Jihadharini msije
mkadanganywa. Maana wengi watakuja
kwa Jina langu, wakidai, 'Mimi ndiye,' na,

[a]**20:36** Yn 1:12; 1Yn 3:1-2
[b]**20:37** Kut 3:6
[c]**20:38** Rum 6:10-11
[d]**20:40** Mt 22:46; Mk 12:34
[e]**20:41** Mt 22:42; Mk 12:35
[f]**20:41** Mt 22:41-45; Mk 12:35-37
[g]41 *Kristo* maana yake ni *Masiya*, yaani *Aliyetiwa mafuta.*
[h]**20:42** Za 110:1; Mdo 2:34
[i]**20:43** Za 110:1; Mt 22:44
[j]**20:45** Lk 11:43
[k]**20:46** Lk 11:43
[l]**20:47** Mt 23:14
[m]**21:1** Mt 27:6; Yn 8:20
[n]**21:3** 2Kor 8:12
[o]**21:4** 2Kor 8:12
[p]**21:6** Lk 19:44
[q]**21:8** Lk 17:23

'Wakati umekaribia.' Msiwafuate. 9 [a]Lakini
msikiapo habari za vita na machafuko,
msiogope. Kwa maana hayo ni lazima
yatokee kwanza, ila ule mwisho hautakuja
wakati huo."
10 [b]Kisha akawaambia: "Taifa litainuka
dhidi ya taifa jingine, na ufalme mmoja
dhidi ya ufalme mwingine. 11 [c]Kutakuwa na
mitetemeko mikubwa ya ardhi, na njaa kali,
na magonjwa ya kuambukiza katika sehemu
mbalimbali. Pia kutakuwa na matukio ya
kutisha na ishara kuu kutoka mbinguni.
12 [d]"Lakini kabla yote hayajatokea,
watawakamata ninyi na kuwatesa.
Watawatia mikononi mwa wakuu wa
masinagogi na kuwafunga magerezani.
Nanyi mtapelekwa mbele ya wafalme na
watawala kwa ajili ya Jina langu. 13 [e]Hii
itawapa nafasi ya kushuhudia. 14 [f]Lakini
kusudieni mioyoni mwenu msisumbuke
awali kuhusu mtakalosema mbele ya
mashtaka. 15 [g]Kwa maana nitawapa maneno
na hekima ambayo hakuna hata adui yenu
mmoja atakayeweza kushindana nayo wala
kuipinga. 16 [h]Mtasalitiwa hata na wazazi,
ndugu, jamaa na marafiki, na baadhi
yenu watawaua. 17 [i]Mtachukiwa na watu
wote kwa ajili ya Jina langu. 18 [j]Lakini
hapatakuwa na unywele mmoja wa kichwa
chenu utakaoangamia. 19 [k]Kwa kuvumilia
mtaokoa roho zenu.

*Kuharibiwa Kwa Yerusalemu Kwatabiriwa*

**(Mathayo 24:15-21; Marko 13:14-19)**

20 [l]"Mtakapoona mji wa Yerusalemu
umezungukwa na majeshi, basi fahamuni
kwamba kuharibiwa kwake kumekaribia.
21 [m]Wakati huo, wale walio Uyahudi
wakimbilie milimani, walio mjini
Yerusalemu watoke humo, nao wale walioko
mashambani wasiingie mjini. 22 [n]Kwa
sababu huu utakuwa ni wakati wa adhabu
ili kutimiza yote yaliyoandikwa. 23 [o]Ole wao
wenye mimba na wale wanaonyonyesha
watoto siku hizo! Kutakuwa na dhiki kuu
katika nchi na ghadhabu juu ya hawa watu.
24 [p]Wataanguka kwa makali ya upanga, na
wengine watachukuliwa kuwa mateka
katika mataifa yote. Nao mji wa Yerusalemu
utakanyagwa na watu wa Mataifa hadi
muda wa hao watu wa Mataifa utimie.

*Kuja Kwa Mwana Wa Adamu*

**(Mathayo 24:29-35; Marko 13:24-31)**

25 [q]"Kutakuwa na ishara katika jua, mwezi
na nyota. Hapa duniani, mataifa yatakuwa
katika dhiki na fadhaa kutokana na
ngurumo na misukosuko ya bahari. 26 [r]Watu
watazimia roho kutokana na hofu kuu na
kuyaona yale mambo yanayotokea duniani,
kwa maana nguvu za angani zitatikisika.
27 [s]Wakati huo ndipo watakapomwona
Mwana wa Adamu akija mawinguni pamoja
na uweza na utukufu mkuu. 28 [t]Mambo
haya yatakapoanza kutendeka, simameni
na mkaviinue vichwa vyenu, kwa sababu
ukombozi wenu umekaribia."
29 [u]Akawaambia mfano huu: "Uangalieni
mtini na miti mingine yote. 30 Inapochipua
majani, ninyi wenyewe mnaweza kuona
na kutambua wenyewe ya kuwa wakati
wa kiangazi umekaribia. 31 [v]Vivyo hivyo,
myaonapo mambo haya yakitukia,
mnatambua kwamba Ufalme wa Mungu
umekaribia.

[a]**21:9** Dan 2:28
[b]**21:10** 2Nya 15:6; Isa 19:2
[c]**21:11** Isa 29:6; Yoe 2:30
[d]**21:12** Lk 12:11; Mk 13:9; Ufu 2:10; Mdo 1:3; 5:18; 12:4; 16:24; 25:23; 1Pet 2:13
[e]**21:13** Flp 1:12
[f]**21:14** Lk 12:11-12
[g]**21:15** Mdo 6:10
[h]**21:16** Lk 12:52-53
[i]**21:17** Yn 15:21
[j]**21:18** Mt 10:30
[k]**21:19** Mt 10:22
[l]**21:20** Lk 19:43
[m]**21:21** Lk 17:31
[n]**21:22** Dan 9:24-27; Hos 9:7; Mk 1:22
[o]**21:23** Mt 24:19
[p]**21:24** Dan 8:13; Ufu 11:2
[q]**21:25** 2Pet 3:10-12
[r]**21:26** Mt 24:29
[s]**21:27** Mt 8:20; Ufu 1:7
[t]**21:28** Lk 18:7
[u]**21:29** Mt 24:32; Mk 12:28
[v]**21:31** Mt 3:2

32 [a]“Amin, nawaambia, kizazi hiki
hakitapita hadi mambo haya yote yawe
yametimia. 33 [b]Mbingu na nchi zitapita,
lakini maneno yangu hayatapita kamwe.”

*Siku Ya Mwisho Itakuja Ghafula*

34 [c]“Jihadharini mioyo yenu isije
ikalemewa na anasa, ulevi na fadhaa za
maisha haya, nayo siku ile ikawakuta ninyi
bila kutazamia kama vile mtego unasavyo.
35 [d]Kwa maana kama vile mtego unasavyo,
ndivyo siku hiyo itakavyowapata wanadamu
wote waishio katika uso wa dunia yote.
36 [e]Kesheni daima na mwombe ili mweze
kuokoka na yale yote yatakayotokea na
kusimama mbele ya Mwana wa Adamu.”

37 [f]Kila siku Yesu alikuwa akifundisha
Hekaluni, na jioni ilipofika, alikwenda
zake kwenye Mlima wa Mizeituni na
kukaa huko usiku kucha. 38 [g]Nao watu wote
walikuja asubuhi na mapema Hekaluni ili
kumsikiliza.

*Yuda Akubali Kumsaliti Yesu*

**(Mathayo 26:14-16; Marko 14:10-11)**

22 [h]Wakati huu Sikukuu ya Mikate
Isiyotiwa Chachu, iitwayo Pasaka,
ilikuwa imekaribia. 2 [i]Viongozi wa makuhani
na walimu wa sheria walikuwa wanatafuta
njia ya kumuua Yesu, kwa sababu
waliwaogopa watu. 3 [jk]Shetani akamwingia
Yuda, aliyeitwa Iskariote, mmoja wa wale
Kumi na Wawili. 4 [l]Yuda akaenda kwa
viongozi wa makuhani na kwa maafisa
wa walinzi wa Hekalu, akazungumza nao
jinsi ambavyo angeweza kumsaliti Yesu.
5 [m]Wakafurahi na wakakubaliana kumpa
fedha. 6 Naye akakubali, akaanza kutafuta
wakati uliofaa wa kumsaliti Yesu kwao,
wakati ambapo hakuna umati wa watu.

*Maandalizi Ya Pasaka*

**(Mathayo 26:17-25; Marko 14:12-21; Yohana 13:21-30)**

7 [n]Basi ikawadia siku ya Mikate Isiyotiwa
Chachu, siku ambayo mwana-kondoo
wa Pasaka huchinjwa. 8 [o]Hivyo Yesu
akawatuma Petro na Yohana, akisema,
“Nendeni mkatuandalie chakula cha Pasaka
ili tuweze kuila.”

9 Wakamuuliza, “Unataka tukuandalie
wapi?”

10 Yesu akawaambia, “Tazameni,
mtakapokuwa mkiingia mjini, mtakutana
na mwanaume amebeba mtungi wa
maji. Mfuateni mpaka kwenye nyumba
atakayoingia. 11 Nanyi mwambieni
mwenye nyumba, ‘Mwalimu anauliza:
Kiko wapi chumba cha wageni, ambamo
mimi na wanafunzi wangu tutakula
Pasaka?’ 12 Atawaonyesha chumba kikubwa
ghorofani, kikiwa kimepambwa vizuri.
Andaeni humo.”

13 [p]Wakaenda, nao wakakuta kila
kitu kama Yesu alivyowaambia. Hivyo
wakaiandaa Pasaka.

*Kuanzishwa Kwa Meza Ya Bwana*

**(Mathayo 26:31-35; Marko 14:27-31; Yohana 13:36-38)**

14 [q]Wakati ulipowadia, Yesu akaketi
mezani pamoja na wale mitume wake.
15 [r]Kisha akawaambia, “Nimetamani sana
kuila Pasaka hii pamoja nanyi kabla
ya kuteswa kwangu. 16 [s]Kwa maana,
nawaambia, sitaila tena Pasaka mpaka
itakapotimizwa katika Ufalme wa Mungu.”

17 Akiisha kukichukua kikombe,
akashukuru, akasema, “Chukueni hiki

---

[a]**21:32** Lk 11:50; 11:25
[b]**21:33** Mt 5:18
[c]**21:34** Mk 4:19; Lk 12:40-46; 1The 5:2-7
[d]**21:35** 1The 5:2; 2Pet 3:10; Ufu 3:3; 16:15
[e]**21:36** Mt 26:41
[f]**21:37** Mt 26:55; 21:1
[g]**21:38** Yn 8:2
[h]**22:1** Yn 11:55
[i]**22:2** Mt 12:14
[j]**22:3** Mt 4:10; Mk 14:10, 11
[k]**22:3** Mt 4:10; Yn 13:2; Mt 10:4
[l]**22:4** Mdo 4:1; 5:24
[m]**22:5** Zek 11:12
[n]**22:7** Kum 16:5-8; Mk 4:12
[o]**22:8** Mdo 3:1, 11; 4:13-19
[p]**22:13** Lk 19:32
[q]**22:14** Mk 6:30; Mt 26:20; Mk 14:17-18
[r]**22:15** Mt 16:21
[s]**22:16** Lk 14:15; Ufu 19:9

mnywe wote. 18 [a]Kwa maana nawaambia
tangu sasa sitakunywa tena katika uzao
wa mzabibu, hadi Ufalme wa Mungu
utakapokuja."
19 [b]Kisha akachukua mkate, akashukuru,
akaumega, na kuwapa, akisema, "Huu ni
mwili wangu unaotolewa kwa ajili yenu.
Fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu."
20 [c]Vivyo hivyo baada ya kula, akakitwaa
kikombe, akisema, "Kikombe hiki ni agano
jipya katika damu yangu, imwagikayo kwa
ajili yenu. 21 [d]Lakini mkono wake huyo
atakayenisaliti uko hapa mezani pamoja
nami. 22 [e]Mwana wa Adamu anaenda zake
kama ilivyokusudiwa. Lakini ole wake mtu
huyo amsalitiye." 23 [f]Wakaanza kuulizana
wenyewe ni nani miongoni mwao angeweza
kufanya jambo hilo.

*Mabishano Kuhusu Ukuu*

24 [g]Pia yakazuka mabishano katikati ya
wanafunzi kwamba ni nani aliyeonekana
kuwa mkuu kuliko wote miongoni mwao.
25 Yesu akawaambia, "Wafalme na watu wa
Mataifa huwatawala watu kwa nguvu. Nao
wenye mamlaka juu yao hujiita 'Wafadhili.'
26 [h]Lakini ninyi msifanane nao. Bali yeye
aliye mkuu kuliko wote miongoni mwenu,
inampasa kuwa kama yeye aliye mdogo
wa wote, naye atawalaye na awe kama
yeye ahudumuye. 27 [i]Kwani ni nani aliye
mkuu? Ni yule aketiye mezani au ni yule
ahudumuye? Si ni yule aliyekaa mezani?
Lakini mimi niko miongoni mwenu kama
yule ahudumuye. 28 [j]Ninyi mmekuwa
pamoja nami katika majaribu yangu.
29 [k]Nami kama Baba yangu alivyonipa
ufalme, kadhalika mimi nami ninawapa
ninyi, 30 ili mpate kula na kunywa mezani
pangu katika karamu ya ufalme wangu,
na kukaa katika viti vya enzi, mkihukumu
makabila kumi na mawili ya Israeli."

*Yesu Atabiri Kuwa Petro Atamkana*

31 [l]Yesu akasema, "Simoni, Simoni,
sikiliza, Shetani ameomba kuwapepeta ninyi
wote kama ngano. 32 [m]Lakini nimekuombea
wewe Simoni ili imani yako isishindwe,
nawe ukiisha kunirudia, uwaimarishe
ndugu zako."
33 [n]Petro akajibu, "Bwana, niko tayari
kwenda pamoja nawe gerezani na hata
kifoni."
34 [o]Yesu akamjibu, "Ninakuambia Petro,
kabla jogoo hajawika usiku wa leo, utakana
mara tatu kwamba hunijui mimi."

*Mfuko, Mkoba Na Upanga*

35 [p]Kisha Yesu akawauliza, "Nilipowatuma
bila mfuko, wala mkoba, wala viatu,
mlipungukiwa na kitu chochote?"
Wakajibu, "La, hatukupungukiwa na kitu
chochote."
36 Akawaambia, "Lakini sasa, aliye na
mfuko na auchukue, na aliye na mkoba
vivyo hivyo. Naye asiye na upanga, auze
joho lake anunue mmoja. 37 [q]Kwa sababu,
nawaambia, andiko hili lazima litimizwe
juu yangu, kwamba, 'Alihesabiwa pamoja
na wakosaji'; kwa kweli yaliyoandikwa
kunihusu mimi hayana budi kutimizwa."
38 Wanafunzi wake wakamwambia,
"Bwana, tazama hapa kuna panga mbili."
Akawajibu, "Inatosha."

*Yesu Aomba Kwenye Mlima Wa Mizeituni*

**(Mathayo 26:36-46; Marko 14:32-42)**

39 [r]Yesu akatoka, akaenda kwenye Mlima
wa Mizeituni kama ilivyokuwa kawaida
yake, nao wanafunzi wake wakamfuata.

---

[a]**22:18** Mt 26:29; Mk 14:29
[b]**22:19** Mt 14:19
[c]**22:20** Zek 9:11; 2Kor 3:6
[d]**22:21** Za 41:9
[e]**22:22** Mt 8:20; Mdo 2:23; 4:29
[f]**22:23** Mt 26:22; Yn 13:22, 25
[g]**22:24** Mk 9:34; Lk 9:46
[h]**22:26** 1Pet 5:5; Mk 9:35; Lk 12:37
[i]**22:27** Mt 20:28; Lk 12:37
[j]**22:28** Ebr 4:15
[k]**22:29** Mt 25:34; 2Tim 2:12
[l]**22:31** Ay 16:12; Amo 9:9
[m]**22:32** Yn 17:9-15; Rum 8:34; Yn 21:15-17
[n]**22:33** Yn 11:16
[o]**22:34** Mt 26:34; Mk 14:30; Yn 13:38
[p]**22:35** Mt 10:9-10; Lk 9:3
[q]**22:37** Isa 53:12
[r]**22:39** Lk 21:37; Mt 21:1

40 [a]Walipofika huko, akawaambia
wanafunzi wake, "Ombeni, msije mkaingia
majaribuni." 41 [b]Akajitenga nao kama umbali
wa kutupa jiwe, akapiga magoti, akaomba
42 [c]akisema, "Baba, kama ni mapenzi yako,
niondolee kikombe hiki. Lakini si kama
nipendavyo, bali mapenzi yako yatendeke."
43 [d]Malaika kutoka mbinguni akamtokea,
akamtia nguvu. 44 [e]Naye akiwa katika
maumivu makuu, akaomba kwa bidii, nalo
jasho lake likawa kama matone ya damu
yakidondoka ardhini.

45 Baada ya kuomba, akawarudia
wanafunzi wake akawakuta wamelala,
wakiwa wamechoka kutokana na huzuni.
46 [f]Naye akawauliza, "Mbona mmelala?
Amkeni, mwombe ili msije mkaingia
majaribuni."

*Yesu Akamatwa*

**(Mathayo 26:47-56; Marko 14:43-50; Yohana 18:3-11)**

47 [g]Yesu alipokuwa bado anazungumza,
umati mkubwa wa watu ukaja. Uliongozwa
na Yuda, ambaye alikuwa mmoja wa wale
wanafunzi Kumi na Wawili. Akamkaribia
Yesu ili ambusu. 48 Lakini Yesu akamwambia,
"Yuda, je, unamsaliti Mwana wa Adamu
kwa busu?"

49 Wafuasi wa Yesu walipoona yale
yaliyokuwa yanakaribia kutokea,
wakasema, "Bwana, tuwakatekate kwa
panga zetu?" 50 [h]Mmoja wao akampiga
mtumishi wa kuhani mkuu kwa upanga,
akamkata sikio la kuume.

51 Lakini Yesu akasema, "Acheni!"
Akaligusa lile sikio la yule mtu na
kumponya.

52 [i]Kisha Yesu akawaambia wale viongozi
wa makuhani, maafisa wa walinzi wa
Hekalu, pamoja na wazee waliokuwa
wamekuja kumkamata, "Mmekuja
na panga na marungu, kana kwamba
mimi ni mnyang'anyi? 53 [j]Siku kwa siku
nilikuwa pamoja nanyi Hekaluni lakini
hamkunikamata. Lakini hii ni saa yenu,
wakati giza linatawala!"

*Petro Amkana Yesu*

**(Mathayo 26:57-75; Marko 14:53-72; Yohana 18:12-27)**

54 [k]Kisha wakamkamata Yesu,
wakamchukua, wakaenda naye mpaka
nyumbani kwa kuhani mkuu. Lakini Petro
akafuata kwa mbali. 55 [l]Walipokwisha
kuwasha moto katikati ya ua na kuketi
pamoja, Petro naye akaketi pamoja nao.
56 Mtumishi mmoja wa kike akamwona
kwa mwanga wa moto akiwa ameketi pale.
Akamtazama sana, akasema, "Huyu mtu pia
alikuwa pamoja na Yesu!"

57 Lakini Petro akakana, akasema, "Ewe
mwanamke, hata simjui!"

58 [m]Baadaye kidogo, mtu mwingine
alimwona Petro akasema, "Wewe pia ni
mmoja wao!" Petro akajibu, "Wewe mtu,
mimi sio mmoja wao!"

59 [n]Baada ya muda wa kama saa moja
hivi, mtu mwingine akazidi kusisitiza, "Kwa
hakika huyu mtu naye alikuwa pamoja na
Yesu, kwa maana yeye pia ni Mgalilaya."

60 Petro akajibu, "Wewe mtu, mimi sijui
unalosema!" Wakati huo huo, akiwa bado
anazungumza, jogoo akawika. 61 [o]Naye
Bwana akageuka, akamtazama Petro. Ndipo
Petro akakumbuka lile neno ambalo Bwana
alimwambia: "Kabla jogoo hajawika leo,
utanikana mara tatu." 62 Naye akaenda nje,
akalia kwa majonzi.

---

[a]**22:40** Mt 6:13; 26:41; Mk 14:38
[b]**22:41** Lk 18:11
[c]**22:42** Mt 20:22; 26:39
[d]**22:43** Mt 4:11; 1:13
[e]**22:44** Yn 12:27
[f]**22:46** Lk 22:40
[g]**22:47** Mt 26:47-57; Mk 14:43-49; Yn 18:2-11
[h]**22:50** Mt 26:51; Mk 14:47; Yn 18:10
[i]**22:52** Mt 26:55; Mk 14:14-48
[j]**22:53** Mt 26:55; Yn 12:27; Mt 8:12; Yn 3:20
[k]**22:54** Mt 26:57; Mk 14:53; Mt 26:58; Yn 18:15
[l]**22:55** Mt 26:69; Mk 14:66
[m]**22:58** Mt 26:71; Mk 14:69; Yn 18:26
[n]**22:59** Lk 23:6
[o]**22:61** Lk 7:13

*Walinzi Wamdhihaki Yesu Na Kumpiga*

**(Mathayo 26:67-68; Marko 14:65)**

63 [ab]Watu waliokuwa wanamlinda Yesu
wakaanza kumdhihaki na kumpiga.
64 Wakamfunga kitambaa machoni na
kumuuliza, "Tabiri! Tuambie ni nani
aliyekupiga?" 65 [c]Wakaendelea kumtukana
kwa matusi mengi.

*Yesu Apelekwa Mbele Ya Baraza*

**(Mathayo 26:59-66; Marko 14:55-64; Yohana 18:28-38)**

66 [d]Kulipopambazuka, baraza la wazee
wa watu,[e] yaani viongozi wa makuhani
na walimu wa sheria, wakakutana
pamoja, naye Yesu akaletwa mbele yao.
67 [f]Wakamwambia, "Kama wewe ndiye
Kristo,[g] tuambie."

Yesu akawajibu, "Hata nikiwaambia
hamtaamini. 68 [h]Nami nikiwauliza swali,
hamtanijibu. 69 [i]Lakini kuanzia sasa, Mwana
wa Adamu ataketi mkono wa kuume wa
Mungu Mwenye Nguvu."

70 [j]Wote wakauliza, "Wewe basi ndiwe
Mwana wa Mungu?"

Yeye akawajibu, "Ninyi mwasema
kwamba mimi ndiye."

71 [k]Kisha wakasema, "Tuna haja gani tena
ya ushahidi zaidi? Tumesikia wenyewe
kutoka kinywani mwake."

*Yesu Apelekwa Kwa Pilato*

**(Mathayo 27:1-14; Marko 15:1-5; Yohana 18:28-38)**

23 [l]Kisha umati wote wa watu ukainuka
na kumpeleka Yesu kwa Pilato.
2 [m]Nao wakaanza kumshtaki wakisema:
"Tumemwona huyu mtu akipotosha taifa
letu, akiwazuia watu wasilipe kodi kwa
Kaisari na kujiita kuwa yeye ni Kristo,[n]
mfalme."

3 [o]Basi Pilato akamuuliza Yesu, "Wewe
ndiye mfalme wa Wayahudi?"

Yesu akajibu, "Wewe wasema."

4 [p]Pilato akawaambia viongozi wa
makuhani na watu wote waliokuwepo,
"Sioni sababu ya kutosha kumshtaki mtu
huyu!"

5 [q]Lakini wao wakakazana kusema,
"Anawachochea watu kwa mafundisho
yake katika Uyahudi yote, tangu Galilaya
alikoanzia, hadi sehemu hii!"

*Yesu Apelekwa Kwa Herode*

6 [r]Pilato aliposikia hayo akauliza, "Huyu
mtu ni Mgalilaya?" 7 [s]Alipofahamu kwamba
Yesu alikuwa chini ya mamlaka ya Herode,
akampeleka kwa Herode, ambaye wakati
huo alikuwa pia Yerusalemu.

8 [t]Herode alipomwona Yesu alifurahi
sana, kwa sababu kwa muda mrefu alikuwa
amesikia mambo mengi kumhusu yeye. Pia
alitarajia kumwona akifanya miujiza kadha
wa kadha. 9 [u]Herode akamuuliza maswali
mengi, lakini Yesu hakumjibu lolote.
10 Wakati huo viongozi wa makuhani na
walimu wa sheria walikuwepo wakitoa
mashtaka yao kwa nguvu sana. 11 [v]Herode
na askari wake wakamdhihaki Yesu na

---

[a]**22:63** Mt 26:67, 68; Mk 14:65
[b]**22:63** Mt 26:67, 68; Mk 14:65
[c]**22:65** Mt 16:21
[d]**22:66** Mt 5:22; 27:1; Mk 15:1; Mdo 4:26; 22:5
[e]66 Baraza la wazee hapa ina maana ya Sanhedrin ambalo lilikuwa ndilo Baraza la juu kabisa la utawala wa Kiyahudi, lililoundwa na wazee 70 pamoja na kuhani mkuu.
[f]**22:67** Mt 26:63; Mk 14:61
[g]67 *Kristo* maana yake ni *Masiya*, yaani *Aliyetiwa mafuta.*
[h]**22:68** Lk 20:3-8
[i]**22:69** Mk 16:19
[j]**22:70** Mt 26:65; 27:11; Lk 23:3
[k]**22:71** Mt 26:65; Mk 14:62

[l]**23:1** Mk 15:1; Yn 18:28
[m]**23:2** Lk 20:22; Yn 18:28
[n]2 *Kristo* maana yake ni *Masiya*, yaani *Aliyetiwa mafuta.*
[o]**23:3** Mt 27:11; 1Tim 6:13
[p]**23:4** 1Tim 6:13; 2Kor 5:21
[q]**23:5** Mk 1:14
[r]**23:6** Lk 22:59
[s]**23:7** Mk 14:1; Lk 3:1
[t]**23:8** Lk 9:9
[u]**23:9** Mk 14:61
[v]**23:11** Mk 15:17-19; Yn 19:2-3

kumfanyia mzaha. Wakamvika vazi zuri
sana, wakamrudisha kwa Pilato. 12 [a]Siku
hiyo, Herode na Pilato wakawa marafiki;
kabla ya jambo hili walikuwa na uadui kati
yao.

*Yesu Ahukumiwa Kifo*

**(Mathayo 27:15-26; Marko 15:6-15; Yohana 18:39–19:16)**

13 [b]Basi Pilato akawaita pamoja viongozi
wa makuhani, viongozi wengine na
watu, 14 [c]akawaambia, “Ninyi mlimleta
huyu mtu kwangu kana kwamba ni mtu
anayewachochea watu ili waasi. Nimemhoji
mbele yenu nami nimeona hakuna msingi
wowote wa mashtaka yenu dhidi yake.
15 Wala Herode hakumwona na kosa
lolote, ndiyo sababu amemrudisha kwetu.
Kama mnavyoona, mtu huyu hakufanya
jambo lolote linalostahili kifo. 16 [d]Kwa hiyo
nitaamuru apigwe mijeledi na kumwachia.”
[ 17 [e]Kwa kuwa ilikuwa lazima kuwafungulia
mfungwa mmoja wakati wa Sikukuu.]

18 [f]Ndipo watu wote wakapiga kelele kwa
pamoja, “Mwondoe mtu huyo! Tufungulie
Baraba!” 19 (Baraba alikuwa amefungwa
gerezani kwa sababu ya maasi yaliyokuwa
yametokea mjini, na kwa ajili ya uuaji.)

20 Pilato, akitaka kumwachia Yesu,
akasema nao tena. 21 Lakini wao
wakaendelea kupiga kelele wakisema,
“Msulubishe! Msulubishe!”

22 [g]Kwa mara ya tatu, Pilato akawauliza,
“Kwani amefanya kosa gani huyu mtu?
Sikuona kwake sababu yoyote inayostahili
adhabu ya kifo. Kwa hiyo nitaamuru apigwe
mijeledi, na kisha nitamwachia.”

23 Lakini watu wakazidi kupiga kelele
kwa nguvu zaidi, wakidai kwamba Yesu
asulubiwe. Hivyo, kelele zao zikashinda.
24 [h]Kwa hiyo Pilato akatoa hukumu kwamba
madai yao yatimizwe. 25 Akamfungua yule
mtu aliyekuwa amefungwa gerezani kwa
kuhusika katika uasi dhidi ya serikali
na mauaji. Akamkabidhi Yesu mikononi
mwao, wamfanyie watakavyo.

*Kusulubiwa Kwa Yesu*

**(Mathayo 27:32-44; Marko 15:21-32; Yohana 19:17-27)**

26 [i]Walipokuwa wakienda naye,
wakamkamata mtu mmoja aitwaye
Simoni mwenyeji wa Kirene, aliyekuwa
anapita zake kuingia mjini kutoka
shambani. Wakambebesha msalaba,
wakamlazimisha auchukue nyuma ya
Yesu. 27 [j]Idadi kubwa ya watu wakamfuata
Yesu, wakiwamo wanawake waliokuwa
wakimlilia na kumwombolezea. 28 [k]Yesu
akawageukia, akawaambia, “Enyi binti za
Yerusalemu, msinililie mimi bali jililieni
ninyi wenyewe na watoto wenu. 29 [l]Kwa
maana wakati utafika mtakaposema,
‘Wamebarikiwa wanawake tasa, ambao
matumbo yao hayakuzaa, wala matiti yao
hayakunyonyesha!’ 30 [m]Ndipo

“ ‘wataiambia milima,
“Tuangukieni!”
na vilima, “Tufunikeni!” ’

31 [n]Kwa maana kama wamefanya hivi kwa
mti mbichi, kwa mti mkavu itakuwaje?”

32 [o]Watu wengine wawili wahalifu,
walipelekwa pamoja na Yesu ili
wakasulubiwe. 33 Walipofika mahali
paitwapo Fuvu la Kichwa, hapo ndipo
walipomsulubisha Yesu pamoja na hao
wahalifu, mmoja upande wake wa kuume
na mwingine upande wake wa kushoto.
34 [p]Yesu akasema, “Baba, wasamehe, kwa
maana hawajui walitendalo!” Wakagawana
nguo zake kwa kupiga kura.

---

[a]**23:12** Mdo 4:27
[b]**23:13** Mt 27:23; Mk 15:14; Yn 18:38
[c]**23:14** Lk 23:1, 2, 4
[d]**23:16** Mdo 16:37; 2Kor 11:23-24
[e]**23:17** Mt 27:15; Mk 15:6; Yn 18:39
[f]**23:18** Mdo 3:13-14
[g]**23:22** Lk 23:18
[h]**23:24** Mt 27:26; Mk 15:15; Yn 19:17
[i]**23:26** Mt 27:32; Mk 15:21; Yn 19:17
[j]**23:27** Lk 8:52
[k]**23:28** Lk 19:41-44; 21:23-24
[l]**23:29** Mt 24:19
[m]**23:30** Hos 10:8; Ufu 6:16
[n]**23:31** Eze 20:47
[o]**23:32** Isa 53:12; Mt 27:38
[p]**23:34** Mt 11:25; 5:44; Za 22:18

35 [a]Watu wakasimama hapo
wakimwangalia, nao viongozi wa Wayahudi
wakamdhihaki wakisema, “Aliokoa
wengine! Ajiokoe mwenyewe basi, kama
yeye ndiye Kristo wa Mungu, Mteule wake.”
36 [b]Askari nao wakaja, wakamdhihaki.
Wakamletea siki ili anywe, 37 [c]na
wakamwambia, “Kama wewe ni Mfalme
wa Wayahudi, jiokoe mwenyewe.”
38 [d]Kwenye msalaba juu ya kichwa chake,
kulikuwa na maandishi haya: HUYU NDIYE
MFALME WA WAYAHUDI.

Maandishi haya yalikuwa yameandikwa kwa lugha za Kiyunani, Kilatini na Kiebrania.

39 [e]Mmoja wa wale wahalifu
waliosulubiwa pamoja naye akamtukana,
akasema: “Wewe si ndiye Kristo? Jiokoe
mwenyewe na utuokoe na sisi.”
40 Lakini yule mhalifu mwingine
akamkemea mwenzake, akasema, “Je, wewe
humwogopi Mungu, wakati uko kwenye
adhabu iyo hiyo? 41 [f]Sisi tumehukumiwa
kwa haki kwa kuwa tunapata tunayostahili
kwa ajili ya matendo yetu. Lakini huyu mtu
hajafanya kosa lolote.”
42 [g]Kisha akasema, “Yesu, unikumbuke
utakapokuja katika Ufalme wako.”
43 [h]Yesu akamjibu, “Amin, nakuambia,
leo hii utakuwa pamoja nami Paradiso.”[i]

*Kifo Cha Yesu*

### (Mathayo 27:45-56; Marko 15:33-41; Yohana 19:28-30)

44 [j]Ilikuwa kama saa sita mchana, nalo
giza likafunika nchi yote hadi saa tisa,
45 [k]kwa sababu jua liliacha kutoa nuru.
Pazia la Hekalu likachanika vipande viwili.
46 [l]Yesu akapaza sauti yake akasema, “Baba,
mikononi mwako naikabidhi roho yangu.”
Baada ya kusema haya, akakata roho.
47 [m]Yule jemadari alipoona yaliyotukia,
akamsifu Mungu, akasema, “Hakika, mtu
huyu alikuwa mwenye haki.” 48 [n]Watu
wote waliokuwa wamekusanyika hapo
kushuhudia tukio hili walipoyaona hayo,
wakapigapiga vifua vyao kwa huzuni
na kwenda zao. 49 [o]Lakini wale wote
waliomfahamu, pamoja na wale wanawake
waliokuwa wamemfuata kutoka Galilaya,
walisimama kwa mbali wakiyatazama
mambo haya.

*Maziko Ya Yesu*

### (Mathayo 27:57-61; Marko 15:42-47; Yohana 19:38-42)

50 [p]Basi kulikuwa na mtu mmoja mwema
na mwenye haki, jina lake Yosefu. Yeye
alikuwa mjumbe wa Baraza la Wayahudi,[q]
51 [r]lakini yeye hakuwa amekubaliana na
maamuzi na vitendo vya viongozi wenzake.
Huyu alikuwa mwenyeji wa Arimathaya
huko Uyahudi, naye alikuwa anaungojea
Ufalme wa Mungu kwa matarajio makubwa.
52 Yosefu alikwenda kwa Pilato, akaomba
apewe mwili wa Yesu. 53 Akaushusha kutoka
msalabani, akaufunga katika kitambaa
cha kitani safi, na kuuweka katika kaburi
lililochongwa kwenye mwamba, ambalo
halikuwa limezikiwa mtu mwingine bado.
54 [s]Ilikuwa Siku ya Maandalizi, nayo Sabato
ilikuwa karibu kuanza.
55 [t]Wale wanawake waliokuwa wamekuja

---

[a]**23:35** Za 22:17; Isa 42:1; Zek 12:10; Mt 27:39; Mk 15:29
[b]**23:36** Za 22:7; 69:21; Mt 27:48
[c]**23:37** Lk 4:3, 9
[d]**23:38** Mt 2:2
[e]**23:39** Mt 27:44; Mk 15:32
[f]**23:41** Lk 23:4
[g]**23:42** Mt 16; 27
[h]**23:43** 1Kor 12:3-4; Ufu 2:7
[i]43 Paradiso maana yake bustani nzuri, hapa ina maana mahali zinapokwenda roho za wacha Mungu, yaani watakatifu.
[j]**23:44** Amo 8:9
[k]**23:45** Kut 26:31-33; Ebr 3:8; 10:19-20
[l]**23:46** Mt 27:50; Za 31:5; 1Pet 2:23; Yn 19:30
[m]**23:47** Mt 9:8
[n]**23:48** Lk 18:13
[o]**23:49** Lk 8:2; Za 38:11
[p]**23:50** Mt 27:59; Mk 15:46
[q]50 *Baraza la Wayahudi* hapa ina maana ya *Sanhedrin* ambalo lilikuwa ndilo baraza la juu kabisa la utawala wa Kiyahudi, lililoundwa na wazee 70 pamoja na kuhani mkuu.
[r]**23:51** Lk 2:25, 38
[s]**23:54** Mt 27:62
[t]**23:55** Lk 8:2; Mk 15:47

pamoja na Yesu wakimfuata kutoka Galilaya wakamfuata Yosefu, wakaliona kaburi na jinsi mwili wa Yesu ulivyolazwa. 56 [a]Kisha wakarudi nyumbani, wakaandaa manukato na marhamu ya kuupaka huo mwili. Lakini wakapumzika siku ya Sabato kama ilivyoamriwa.

*Kufufuka Kwa Yesu*

**(Mathayo 28:1-10; Marko 16:1-8; Yohana 20:1-10)**

24 [b]Mnamo siku ya kwanza ya juma, alfajiri na mapema, wale wanawake walichukua yale manukato waliyokuwa wameyaandaa, wakaenda kaburini. 2 [c]Wakakuta lile jiwe limevingirishwa kutoka kwenye kaburi, 3 [d]lakini walipoingia ndani, hawakuuona mwili wa Bwana Yesu. 4 [e]Walipokuwa wanashangaa juu ya jambo hili, ghafula watu wawili waliokuwa wamevaa mavazi yanayong'aa kama umeme wakasimama karibu nao. 5 Wale wanawake, wakiwa na hofu, wakainamisha nyuso zao mpaka chini. Lakini wale watu wakawaambia, “Kwa nini mnamtafuta aliye hai miongoni mwa wafu? 6 [f]Hayuko hapa; amefufuka! Kumbukeni alivyowaambia alipokuwa bado yuko pamoja nanyi huko Galilaya kwamba: 7 [g]‘Ilikuwa lazima Mwana wa Adamu atiwe mikononi mwa watu wenye dhambi na waovu ili asulubiwe, na siku ya tatu afufuke.’ ” 8 [h]Ndipo wakayakumbuka maneno ya Yesu.

9 [i]Waliporudi kutoka huko kaburini, wakawaeleza wale wanafunzi kumi na mmoja pamoja na wengine wote mambo haya yote. 10 [j]Basi Maria Magdalene, Yoana, na Maria mama yake Yakobo, pamoja na wanawake wengine waliofuatana nao ndio waliwaelezea mitume habari hizi. 11 [k]Lakini hawakuwasadiki hao wanawake, kwa sababu maneno yao yalionekana kama upuzi. 12 [l]Hata hivyo, Petro akainuka na kukimbia kwenda kule kaburini. Alipoinama kuchungulia, akaona vile vitambaa vya kitani, ila hakuona kitu kingine. Naye akaenda zake akijiuliza nini kilichotokea.

*Njiani Kwenda Emau*

**(Marko 16:12-13)**

13 [m]Ikawa siku iyo hiyo, wanafunzi wawili wa Yesu walikuwa njiani wakienda kijiji kilichoitwa Emau, yapata maili saba[n] kutoka Yerusalemu. 14 Walikuwa wakizungumza wao kwa wao kuhusu mambo yote yaliyotukia. 15 [o]Walipokuwa wakizungumza na kujadiliana, Yesu mwenyewe akaja akatembea pamoja nao, 16 [p]lakini macho yao yakazuiliwa ili wasimtambue.

17 Akawauliza, “Ni mambo gani haya mnayozungumza wakati mnatembea?”

Wakasimama, nyuso zao zikionyesha huzuni. 18 [q]Mmoja wao, aliyeitwa Kleopa, akamuuliza, “Je, wewe ndiye peke yako mgeni huku Yerusalemu ambaye hufahamu mambo yaliyotukia humo siku hizi?”

19 [r]Akawauliza, “Mambo gani?”

Wakamjibu, “Mambo ya Yesu wa Nazareti. Yeye alikuwa nabii, mwenye uwezo mkuu katika maneno yake na matendo yake, mbele za Mungu na mbele ya wanadamu wote. 20 [s]Viongozi wa makuhani na viongozi wetu walimtoa ahukumiwe kufa, nao wakamsulubisha. 21 [t]Lakini tulikuwa tumetegemea kwamba yeye ndiye angelikomboa Israeli. Zaidi ya hayo, leo ni siku ya tatu tangu mambo haya yatokee. 22 [u]Isitoshe, baadhi ya wanawake katika

[a]**23:56** Mk 16:1; Lk 24:1; Kut 12:16; 20:11
[b]**24:1** Lk 23:56; Mt 28:1; Mk 16; 1; Yn 20:2
[c]**24:2** Mt 24:2; Mk 16:5
[d]**24:3** Lk 24:23; Mk 16:5
[e]**24:4** Yn 20:12; Mdo 1:10
[f]**24:6** Mt 17:22-23; Mk 9:30-31
[g]**24:7** Mt 8:20; 16:21
[h]**24:8** Yn 2:22
[i]**24:9** Mt 28:8; Mk 16:10
[j]**24:10** Lk 8:1-3; Mk 6:30
[k]**24:11** Mk 16:11
[l]**24:12** Yn 20:3-7; 20:10
[m]**24:13** Mk 16:12
[n]13 Maili saba ni kama kilomita 11.2.
[o]**24:15** Mt 18:20
[p]**24:16** Yn 20:14; 21:4
[q]**24:18** Yn 19:25
[r]**24:19** Mk 1:24
[s]**24:20** Lk 23:13
[t]**24:21** Lk 1:68; 2:38; Mt 16:21
[u]**24:22** Mt 28:8; Mk 16:10; Lk 24:9, 10; Yn 20:18

kundi letu wametushtusha. Walikwenda
kaburini leo alfajiri, 23 lakini hawakuukuta
mwili wake. Walirudi wakasema wameona
maono ya malaika ambao waliwaambia
kwamba Yesu yu hai. 24 [a]Kisha baadhi ya
wenzetu walikwenda kaburini wakalikuta
kama vile wale wanawake walivyokuwa
wamesema, lakini yeye hawakumwona."
25 Yesu akawaambia, "Ninyi ni wajinga
kiasi gani, nanyi ni wazito mioyoni mwenu
kuamini mambo yote yaliyonenwa na
manabii! 26 [b]Je, haikumpasa Kristo[c] kuteswa
kwa njia hiyo na kisha aingie katika utukufu
wake?" 27 [d]Naye akianzia na Sheria ya Mose
na Manabii wote, akawafafanulia jinsi
Maandiko yalivyosema kumhusu yeye.
28 [e]Nao walipokaribia kile kijiji
walichokuwa wakienda, Yesu akawa kama
anaendelea mbele. 29 [f]Lakini wao wakamsihi
sana akae nao, wakisema, "Kaa hapa nasi,
kwa maana sasa ni jioni na usiku unaingia."
Basi akaingia ndani kukaa nao.
30 [g]Alipokuwa mezani pamoja nao,
akachukua mkate, akashukuru, akaumega,
akaanza kuwagawia. 31 [h]Ndipo macho yao
yakafumbuliwa, nao wakamtambua, naye
akatoweka machoni pao. Hawakumwona
tena. 32 [i]Wakaulizana wao kwa wao, "Je,
mioyo yetu haikuwakawaka kwa furaha
ndani yetu alipokuwa anazungumza nasi
njiani na kutufafanulia Maandiko?"
33 Wakaondoka mara, wakarudi
Yerusalemu. Wakawakuta wale wanafunzi
kumi na mmoja na wale waliokuwa pamoja
nao, wamekusanyika 34 [j]wakisema, "Ni
kweli! Bwana amefufuka, naye amemtokea
Simoni." 35 [k]Kisha wale wanafunzi wawili
wakaeleza yaliyotukia njiani na jinsi
walivyomtambua Yesu alipoumega mkate.

*Yesu Awatokea Wanafunzi Wake*

**(Mathayo 28:16-20; Marko 16:14-18; Yohana 20:19-23; Matendo 1:6-8)**

36 [l]Walipokuwa bado wanazungumza
hayo, Yesu mwenyewe akasimama katikati
yao, akasema, "Amani iwe nanyi!"
37 [m]Wakashtuka na kuogopa wakidhani
kwamba wameona mzuka. 38 Lakini Yesu
akawauliza, "Kwa nini mnaogopa? Kwa nini
mna shaka mioyoni mwenu? 39 [n]Tazameni
mikono yangu na miguu yangu, mwone
kuwa ni mimi hasa. Niguseni mwone; kwa
maana mzuka hauna nyama na mifupa,
kama mnionavyo kuwa navyo."
40 Aliposema haya, akawaonyesha
mikono na miguu yake. 41 [o]Wakashindwa
kuamini kwa ajili ya furaha na mshangao
waliokuwa nao. Akawauliza, "Mna chakula
chochote hapa?"
42 Wakampa kipande cha samaki
aliyeokwa, 43 [p]naye akakichukua na kukila
mbele yao.
44 [q]Akawaambia, "Haya ndiyo yale
niliyowaambia nilipokuwa bado niko
pamoja nanyi, kwamba yote yaliyoandikwa
kunihusu mimi katika Sheria ya Mose,
Manabii na Zaburi hayana budi kutimizwa."
45 [r]Ndipo akafungua fahamu zao ili waweze
kuyaelewa Maandiko. 46 [s]Akawaambia,
"Haya ndiyo yaliyoandikwa: Kristo
atateswa na siku ya tatu atafufuka kutoka
kwa wafu. 47 [t]Toba na msamaha wa dhambi
zitatangaziwa mataifa yote kupitia jina lake
kuanzia Yerusalemu. 48 [u]Ninyi ni mashahidi
wa mambo haya.

---

[a]**24:24** Lk 24:12; Yn 20:3-19
[b]**24:26** Ebr 2:10; 1Pet 1:11
[c]26 *Kristo* maana yake ni *Masiya,* yaani *Aliyetiwa mafuta.*
[d]**24:27** Mwa 3:15; Hes 2:19; Mk 7:20; Mal 3:1; Yn 1:45
[e]**24:28** Mwa 32:26; 42:7; Mk 6:49
[f]**24:29** Mwa 19:3; Mdo 16:15
[g]**24:30** Mt 14:19
[h]**24:31** Za 39:3; Lk 24:16
[i]**24:32** Za 39:3; Lk 24:27, 28
[j]**24:34** 1Kor 15:5
[k]**24:35** Lk 24:30, 31

[l]**24:36** Yn 20:19, 21, 26; 14:27
[m]**24:37** Mk 6:49
[n]**24:39** Yn 20:27; 1Yn 1:1
[o]**24:41** Mwa 45:26; Yn 21:5
[p]**24:43** Mdo 10:40
[q]**24:44** Lk 24:26; Mt 1:22; 16:21; Za 110
[r]**24:45** Mdo 16:14
[s]**24:46** Lk 24:26; Isa 50:6; 53:2
[t]**24:47** Mdo 10:43; 13:38; Mt 28:19; Mk 13:10
[u]**24:48** Yn 15:27; 1Pet 5:1

*Kuahidiwa Kwa Roho Mtakatifu*

49 [a]"Tazama nitawatumia ahadi ya Baba yangu; lakini kaeni humu mjini hadi mtakapovikwa uwezo utokao juu."

*Kupaa Kwa Yesu Mbinguni*

**(Marko 16:19-20; Matendo 1:9-11)**

50 [b]Akiisha kuwaongoza mpaka kwenye
viunga vya Bethania, akainua mikono
yake juu na kuwabariki. 51 [c]Alipokuwa
anawabariki, akawaacha, akachukuliwa
mbinguni. 52 [d]Kisha wakamwabudu na
kurudi Yerusalemu wakiwa wamejawa na
furaha kuu. 53 [e]Nao wakadumu ndani ya
Hekalu wakimtukuza Mungu. Amen.

---

[a]**24:49** Yn 14:16; Mdo 1:4
[b]**24:50** Mt 21:11
[c]**24:51** 2Fal 2:11
[d]**24:52** Mt 28:9, 17
[e]**24:53** Mdo 2:46

# YOHANA

*Neno Alifanyika Mwili*

1 [a]Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo
Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye
Neno alikuwa Mungu. 2 [b]Tangu mwanzo
huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu.
3 [c]Vitu vyote viliumbwa kwa yeye, wala
pasipo yeye hakuna chochote kilichoumbwa
ambacho kimeumbwa. 4 [d]Ndani yake ndimo
ulimokuwa uzima na huo uzima ulikuwa
nuru ya watu. 5 [e]Nuru hung'aa gizani nalo
giza halikuishinda.
6 [f]Alikuja mtu mmoja aliyetumwa kutoka
kwa Mungu, jina lake Yohana. 7 [g]Alikuja
kama shahidi apate kuishuhudia hiyo nuru,
ili kwa kupitia kwake watu wote waweze
kuamini. 8 [h]Yeye mwenyewe hakuwa ile
nuru, bali alikuja kuishuhudia hiyo nuru.
9 [i]Kwamba nuru halisi, imwangaziayo kila
mtu ilikuwa inakuja ulimwenguni.
10 [j]Huyo Neno alikuwako ulimwenguni
na ingawa ulimwengu uliumbwa kupitia
kwake, haukumtambua. 11 [k]Alikuja kwa
walio wake, lakini wao hawakumpokea.
12 [l]Bali wote waliompokea, aliwapa uwezo
wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio
wale waliaminio jina lake. 13 [m]Hawa ndio
wasiozaliwa kwa damu, wala kwa mapenzi
ya mwili au kwa mapenzi ya mtu, bali kwa
mapenzi ya Mungu.
14 [n]Neno alifanyika mwili, akakaa
miongoni mwetu, nasi tukauona utukufu
wake, utukufu kama wa Mwana pekee
atokaye kwa Baba, amejaa neema na kweli.
15 [o]Yohana alishuhudia habari zake,
akapaza sauti, akisema, "Huyu ndiye yule
niliyewaambia kwamba, 'Yeye ajaye baada
yangu ni mkuu kuniliko mimi, kwa kuwa
alikuwepo kabla yangu.' " 16 [p]Kutokana na
ukamilifu wake, sisi sote tumepokea neema
juu ya neema. 17 [q]Kwa kuwa sheria ilitolewa
kwa mkono wa Mose, lakini neema na kweli
imekuja kupitia Yesu Kristo. 18 Hakuna mtu
yeyote aliyemwona Mungu wakati wowote,
ila ni Mungu Mwana pekee, aliye kifuani
mwa Baba ndiye ambaye amemdhihirisha.

*Ushuhuda Wa Yohana Mbatizaji*

**(Mathayo 3:1-12; Marko 1:1-8; Luka 3:1-18)**

19 [r]Huu ndio ushuhuda wa Yohana wakati
Wayahudi walipowatuma makuhani na
Walawi kutoka Yerusalemu kumuuliza,
"Wewe ni nani?" 20 [s]Yohana alikiri waziwazi
pasipo kuficha akasema, "Mimi si Kristo."[t]
21 [u]Wakamuuliza, "Wewe ni nani basi?
Je, wewe ni Eliya?"

Yeye akajibu, "Hapana, mimi siye."

"Je, wewe ni yule Nabii?"

Akajibu, "Hapana."

22 Ndipo wakasema, "Basi tuambie wewe
ni nani ili tupate jibu la kuwapelekea wale
waliotutuma. Wewe wasemaje juu yako
mwenyewe?"
23 [v]Akawajibu kwa maneno ya nabii Isaya,
akisema, "Mimi ni sauti ya mtu aliaye
nyikani, 'Yanyoosheni mapito ya Bwana.' "
24 Basi walikuwa wametumwa watu

---

[a]**1:1** 1Yn 1:2; Yn 17:5; Flp 2:6; Isa 55:11
[b]**1:2** Ufu 1:8; Mwa 1:1
[c]**1:3** Kol 1:16; Ebr 1:2
[d]**1:4** 1Yn 5:20; Ufu 1:8; Yn 12:46
[e]**1:5** Yn 3:19
[f]**1:6** Mt 3:1
[g]**1:7** Yn 3:26; 5:33; 3:15
[h]**1:8** Yn 1:20
[i]**1:9** 1Yn 2:8; Isa 49:6
[j]**1:10** Yn 1:3; Ebr 1:2; 11; 3
[k]**1:11** Lk 19:14; Mdo 3:26; 13:46
[l]**1:12** Isa 56:5; Rum 8:15; Gal 3:26; 2Pet 1:4; 1Yn 3:1
[m]**1:13** Tit 3:5; Yak 1:18
[n]**1:14** 1Yn 1:1-2; 4:2; Yn 14:6
[o]**1:15** Yn 1:32; 3:32; 5:33; Mt 3:11; Mk 1:7; Lk 3:16; Yn 1:27, 30; 3:31; 8:58; Kol 1:17
[p]**1:16** Kol 1:19; 2:9
[q]**1:17** Kum 32:46
[r]**1:19** Yn 7:1; 10:24
[s]**1:20** Yn 3:28; Lk 3:15-16
[t]20 *Kristo* maana yake ni *Masiya,* yaani *Aliyetiwa mafuta.*
[u]**1:21** Kum 18:15; Mt 11:4
[v]**1:23** Mt 3:1; Isa 40:3

kutoka kwa Mafarisayo 25 [a]wakamuuliza, “Kama wewe si Kristo, wala si Eliya na wala si yule Nabii, kwa nini basi unabatiza?”

26 [b]Yohana akawajibu, “Mimi ninabatiza kwa maji,[c] lakini katikati yenu yupo mtu msiyemjua. 27 [d]Yeye ajaye baada yangu, sistahili hata kufungua kamba za viatu vyake.”

28 [e]Mambo haya yote yalitukia huko Bethania, ng’ambo ya Mto Yordani, mahali Yohana alipokuwa akibatiza.

*Yesu Mwana-Kondoo Wa Mungu*

29 [f]Siku iliyofuata, Yohana alimwona Yesu akimjia akasema, “Tazama, Mwana-Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu! 30 [g]Huyu ndiye yule niliyewaambia kwamba, ‘Mtu anakuja baada yangu ambaye ni mkuu kuniliko mimi, kwa kuwa alikuwepo kabla yangu.’ 31 [h]Mimi mwenyewe sikumfahamu, lakini sababu ya kuja nikibatiza kwa maji ni ili yeye apate kufunuliwa kwa Israeli.”

32 [i]Kisha Yohana akatoa ushuhuda huu: “Nilimwona Roho akishuka kutoka mbinguni kama hua, akakaa juu yake. 33 [j]Mimi nisingemtambua, lakini yeye aliyenituma nibatize kwa maji alikuwa ameniambia, ‘Yule mtu utakayemwona Roho akimshukia na kukaa juu yake, huyo ndiye atakayebatiza kwa Roho Mtakatifu.’ 34 [k]Mimi mwenyewe nimeona jambo hili na ninashuhudia kuwa huyu ndiye Mwana wa Mungu.”

*Wanafunzi Wa Kwanza Wa Yesu*

35 [l]Siku iliyofuata, Yohana alikuwa huko tena pamoja na wanafunzi wake wawili. 36 [m]Alipomwona Yesu akipita, akasema, “Tazama, Mwana-Kondoo wa Mungu!”

37 Wale wanafunzi wawili walipomsikia Yohana akisema haya, wakamfuata Yesu. 38 [n]Yesu akageuka, akawaona wakimfuata akawauliza, “Mnataka nini?”

Wakamwambia, “Rabi,” (maana yake Mwalimu), “Unaishi wapi?”

39 Yesu akawajibu, “Njooni, nanyi mtapaona!”

Hivyo wakaenda na kupaona mahali alipokuwa anaishi, wakakaa naye siku ile, kwa kuwa ilikuwa yapata saa kumi.

40 [o]Andrea nduguye Simoni Petro, alikuwa mmoja wa wale wawili waliosikia yale Yohana aliyokuwa amesema, naye ndiye alimfuata Yesu. 41 [p]Kitu cha kwanza Andrea alichofanya ni kumtafuta Simoni nduguye na kumwambia, “Tumemwona Masiya” (yaani, Kristo). 42 [q]Naye akamleta kwa Yesu.

Yesu akamwangalia na kusema, “Wewe ni Simoni mwana wa Yohana. Utaitwa Kefa” (ambalo limetafsiriwa Petro[r]).

*Yesu Awaita Filipo Na Nathanaeli*

43 [s]Siku iliyofuata Yesu aliamua kwenda Galilaya. Akamkuta Filipo, akamwambia, “Nifuate.”

44 [t]Basi Filipo alikuwa mwenyeji wa Bethsaida, mji alikotoka Andrea na Petro. 45 [u]Filipo naye akamkuta Nathanaeli na kumwambia, “Tumemwona yeye ambaye Mose aliandika habari zake katika Sheria na ambaye pia manabii waliandika kumhusu, yaani, Yesu wa Nazareti, mwana wa Yosefu.”

46 [v]Nathanaeli akauliza, “Nazareti! Je, kitu chochote chema chaweza kutoka

[a]**1:25** Mt 21:25
[b]**1:26** Mt 3:11; Mk 1:7, 8
[c]26 Hapa tafsiri zingine zinasema ndani ya maji.
[d]**1:27** Yn 3:26; Mdo 13:25
[e]**1:28** Yn 3:26; 10:40
[f]**1:29** Mwa 22:8; Ufu 5:6
[g]**1:30** Yn 15:27
[h]**1:31** Mal 3:1; Mt 3:6; Lk 1:17, 76, 77; 3:3, 4
[i]**1:32** Mt 3:16; Mk 1:10
[j]**1:33** Mk 1:4; Mt 3:11
[k]**1:34** Mt 4:3
[l]**1:35** Mt 3:1
[m]**1:36** Yn 1:29
[n]**1:38** Mt 23:7
[o]**1:40** Mt 4:18-22
[p]**1:41** Yn 4:25
[q]**1:42** Mwa 32:28; Mt 16:18
[r]42 Petro kwa Kiyunani au Kefa kwa Kiaramu; maana yake ni Kipande cha mwamba.
[s]**1:43** Mt 10:3; Yn 14:8-9; Mt 4:9
[t]**1:44** Yn 12:21
[u]**1:45** Yn 21:2; Lk 24:27; Mt 2:23; Lk 3:23
[v]**1:46** Yn 7:41-42, 52

Nazareti?” Filipo akamwambia, “Njoo
uone.”
47 [a]Yesu alipomwona Nathanaeli
anakaribia, akanena habari zake akasema,
“Tazama huyu ni Mwisraeli kweli kweli;
hana hila ndani yake.”
48 Nathanaeli akamuuliza,
“Umenifahamuje?”
Yesu akamjibu, “Nilikuona ulipokuwa
bado uko chini ya mtini, kabla hata Filipo
hajakuita.”
49 [b]Nathanaeli akamwambia, “Rabi, wewe
ni Mwana wa Mungu! Wewe ni Mfalme
wa Israeli!”
50 Yesu akamwambia, “Unaamini kwa
kuwa nilikuambia nilikuona ulipokuwa
bado uko chini ya mtini? Basi utaona
mambo makuu zaidi kuliko hilo.” 51 [c]Ndipo
akawaambia, “Amin, amin nawaambia,
ninyi mtaona mbingu ikifunguka na malaika
wa Mungu wakipanda na kushuka juu ya
Mwana wa Adamu.”

*Arusi Huko Kana*

2 [d]Siku ya tatu kulikuwa na arusi katika
mji wa Kana ya Galilaya, naye mama
yake Yesu alikuwepo pale. 2 Yesu pamoja
na wanafunzi wake walikuwa wamealikwa
arusini pia. 3 Divai ilipokwisha, mama yake
Yesu akamwambia, “Wameishiwa na divai.”
4 [e]Yesu akamwambia, “Mwanamke, nina
nini nawe? Saa yangu haijawadia.”
5 [f]Mama yake akawaambia wale
watumishi, “Lolote atakalowaambia,
fanyeni.”
6 [g]Basi ilikuwepo mitungi sita ya
kuhifadhia maji iliyotengenezwa kwa
mawe kwa ajili ya kujitakasa kwa desturi ya
Kiyahudi; kila mtungi ungeweza kuchukua
vipipa viwili au vitatu.[h]
7 Yesu akawaambia wale watumishi,
“Ijazeni hiyo mitungi maji.” Nao wakaijaza
ile mitungi mpaka juu.
8 Kisha akawaambia, “Sasa choteni hayo
maji kidogo, mpelekeeni mkuu wa meza.”
Hivyo wakachota, wakampelekea.
9 [i]Yule mkuu wa meza akayaonja yale
maji ambayo yalikuwa yamebadilika kuwa
divai. Hakujua divai hiyo ilikotoka ingawa
wale watumishi waliochota yale maji wao
walifahamu. Basi akamwita bwana arusi
kando 10 akamwambia, “Watu wote hutoa
kwanza divai nzuri, kisha huleta ile divai
hafifu wageni wakisha kunywa vya kutosha,
lakini wewe umeiweka ile nzuri kupita zote
mpaka sasa.”
11 [j]Huu, ndio uliokuwa muujiza wa
kwanza Yesu aliofanya Kana ya Galilaya.
Hivyo Yesu alidhihirisha utukufu wake, nao
wanafunzi wake wakamwamini.

*Yesu Atakasa Hekalu*

**(Mathayo 21:12-13; Marko 11:15-17; Luka 19:45-46)**

12 Baada ya hayo, Yesu pamoja na mama
yake, ndugu zake na wanafunzi wake,
walishuka mpaka Kapernaumu, wakakaa
huko siku chache.
13 [k]Ilipokaribia wakati wa Pasaka
ya Wayahudi, Yesu alipanda kwenda
Yerusalemu. 14 [lm]Huko Hekaluni aliwakuta
watu wakiuza ng’ombe, kondoo na njiwa,
nao wengine walikuwa wameketi mezani
wakibadili fedha. 15 Akatengeneza mjeledi
kutokana na kamba, akawafukuza wote
kutoka kwenye eneo la Hekalu, pamoja na
kondoo na ng’ombe. Akazipindua meza za
wale wabadili fedha na kuzimwaga fedha
zao. 16 [n]Akawaambia wale waliokuwa
wakiuza njiwa, “Waondoeni hapa!
Mnathubutuje kuifanya nyumba ya Baba
yangu kuwa mahali pa biashara?”

---

[a]**1:47** Za 32:2; Rum 9:4-6
[b]**1:49** Mt 23:7; 4:3; 2; 2; 27:42
[c]**1:51** Mt 3:16; 8:20; Mwa 28:12
[d]**2:1** Yn 4:46; 21:2; Mt 12:46
[e]**2:4** Yn 19:26; Mt 8:26; 26:18; Yn 7:6
[f]**2:5** Mwa 41:55
[g]**2:6** Mk 7:3-4; Yn 3:25
[h]6 Kipipa kimoja chenye ujazo wa lita 40; hivyo kila mtungi ulikuwa na ujazo wa lita 80 au 120.
[i]**2:9** Yn 4:46
[j]**2:11** Mt 12:38; Yn 1:14; Kut 14:31
[k]**2:13** Yn 11:55; Kum 16:1-6; Lk 2:41
[l]**2:14** Mt 21:12; Mk 11:15; Lk 19:45
[m]**2:14** Mt 21:12, 13; Mk 11:15-17; Lk 19:45, 46
[n]**2:16** Lk 2:49

17 [a]Wanafunzi wake wakakumbuka kuwa
imeandikwa: "Wivu wa nyumba yako
utanila."
18 [b]Ndipo Wayahudi wakamuuliza,
"Unaweza kutuonyesha ishara gani ili
kuthibitisha mamlaka uliyo nayo ya
kufanya mambo haya?"
19 [c]Yesu akawajibu, "Libomoeni hili
Hekalu, nami nitalijenga tena kwa siku
tatu!"
20 Wale Wayahudi wakamjibu, "Hekalu
hili lilijengwa kwa muda wa miaka
arobaini na sita, nawe wasema utalijenga
kwa siku tatu?" 21 [d]Lakini yeye Hekalu
alilozungumzia ni mwili wake. 22 [e]Baada
ya kufufuliwa kutoka kwa wafu, wanafunzi
wake wakakumbuka yale aliyokuwa
amesema. Ndipo wakayaamini Maandiko
na yale maneno Yesu aliyokuwa amesema.
23 [f]Ikawa Yesu alipokuwa Yerusalemu
kwenye Sikukuu ya Pasaka, watu wengi
waliona ishara na miujiza aliyokuwa
akifanya, wakaamini katika jina lake.
24 Lakini Yesu hakujiaminisha kwao
kwa sababu aliwajua wanadamu wote.
25 [g]Hakuhitaji ushuhuda wa mtu yeyote
kuhusu mtu, kwa kuwa alijua yote
yaliyokuwa moyoni mwa mtu.

*Nikodemo Amwendea Yesu Usiku*

3 [h]Basi palikuwa na mtu mmoja Farisayo,
jina lake Nikodemo, mmoja wa Baraza la
Wayahudi[i] lililotawala. 2 [j]Huyu alimjia Yesu
usiku akamwambia, "Rabi, tunajua kuwa
wewe ni mwalimu uliyetumwa na Mungu,
kwa maana hakuna mtu awezaye kufanya
miujiza hii uifanyayo wewe, kama Mungu
hayuko pamoja naye."
3 [k]Yesu akamjibu, "Amin, amin
nakuambia, hakuna mtu anayeweza kuuona
Ufalme wa Mungu kama hajazaliwa mara
ya pili."
4 Nikodemo akauliza, "Awezaje mtu
kuzaliwa wakati akiwa mzee? Hakika
hawezi kuingia mara ya pili kwenye tumbo
la mama yake ili azaliwe!"
5 [l]Yesu akamwambia, "Amin, amin
nakuambia, hakuna mtu yeyote anayeweza
kuingia Ufalme wa Mungu kama hajazaliwa
kwa maji na kwa Roho. 6 [m]Mwili huzaa
mwili, lakini Roho huzaa roho. 7 Kwa
hiyo usishangae ninapokuambia huna budi
'kuzaliwa mara ya pili.' 8 [n]Upepo huvuma
popote upendapo. Mvumo wake unausikia
lakini huwezi ukafahamu utokako wala
uendako. Ndivyo ilivyo kwa kila mtu
aliyezaliwa na Roho."
9 [o]Nikodemo akamuuliza, "Mambo haya
yanawezekanaje?"
10 [p]Yesu akamwambia, "Wewe ni
mwalimu mashuhuri wa Waisraeli, nawe
huelewi mambo haya? 11 [q]Amin, amin
ninakuambia, sisi tunazungumza lile
tunalolijua na tunashuhudia lile tulililoliona.
Lakini ninyi watu hamkubali ushuhuda
wetu. 12 [r]Nimewaambia mambo ya duniani,
nanyi hamkuniamini, mtaniaminije basi
nitakapowaambia mambo ya mbinguni?
13 [s]Hakuna mtu yeyote aliyekwenda
mbinguni isipokuwa yeye aliyeshuka
kutoka mbinguni, yaani, Mwana wa
Adamu. 14 [t]Kama vile Mose alivyomwinua
yule nyoka kule jangwani, vivyo hivyo
Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa
juu. 15 [u]Ili kila mtu amwaminiye awe na
uzima wa milele.
16 [v]"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda

[a]**2:17** Za 69; 9
[b]**2:18** Mt 12:38
[c]**2:19** Mt 26:61; Mdo 6:14
[d]**2:21** 1Kor 6:19
[e]**2:22** Lk 24:5-8; Yn 14:26
[f]**2:23** Yn 3:15
[g]**2:25** Kum 31:21; Mt 9:4
[h]**3:1** Yn 7:50; 19:39; Lk 23:13
[i]1 Baraza la Wayahudi hapa ina maana ya Sanhedrin ambalo lilikuwa ndilo Baraza la juu kabisa la utawala wa Kiyahudi, lililoundwa na wazee 70 pamoja na kuhani mkuu.
[j]**3:2** Yn 2:11; 9:16, 33; Mdo 2:22; 10:38
[k]**3:3** Yn 1:13; 1Pet 1:23
[l]**3:5** Tit 3:5
[m]**3:6** Yn 1:13; Mwa 5:3; Za 51:5
[n]**3:8** Mk 4:41; Mhu 11:5
[o]**3:9** Yn 6:52, 60
[p]**3:10** Lk 2:46
[q]**3:11** Yn 1:18; 7:16-17
[r]**3:12** Lk 22:67
[s]**3:13** Mit 30:4; Efe 4:8-10; Ebr 4:14; 9:24
[t]**3:14** Hes 21:8-9; Yn 8:28; 12:32
[u]**3:15** Mwa 15:6; Rum 3:22
[v]**3:16** Rum 5:8; Efe 2:4; Yn 6:29, 40; 11:25-26

ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa
pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee,
bali awe na uzima wa milele. 17 [a]Kwa maana
Mungu hakumtuma Mwanawe kuuhukumu
ulimwengu, bali kupitia kwake ulimwengu
upate kuokolewa. 18 [b]Yeyote amwaminiye
hahukumiwi, lakini asiyeamini amekwisha
kuhukumiwa, kwa sababu hakuliamini
jina la Mwana pekee wa Mungu. 19 [c]Hii
ndiyo hukumu kwamba: Nuru imekuja
ulimwenguni, nao watu wakapenda giza
kuliko nuru kwa sababu matendo yao ni
maovu. 20 [d]Kwa kuwa kila atendaye maovu
huchukia nuru, wala haji kwenye nuru
ili matendo yake maovu yasifichuliwe.
21 Lakini yule aishiye kwa ukweli huja
kwenye nuru, ili ionekane wazi kwamba
matendo yake yametendeka katika Mungu."

*Ushuhuda Wa Yohana Mbatizaji Kuhusu Yesu*

22 [e]Baada ya haya, Yesu na wanafunzi
wake walikwenda katika nchi ya Uyahudi,
nao wakakaa huko kwa muda na kubatiza.
23 [f]Yohana naye alikuwa akibatiza huko
Ainoni karibu na Salimu kwa sababu
huko kulikuwa na maji tele. Watu wazima
wakamjia huko ili kubatizwa. 24 [g](Hii
ilikuwa kabla Yohana hajatiwa gerezani).
25 [h]Mashindano yakazuka kati ya baadhi
ya wanafunzi wa Yohana na Myahudi
mmoja kuhusu suala la desturi ya kunawa
kwa utakaso. 26 [i]Wakamwendea Yohana
wakamwambia, "Rabi, yule mtu aliyekuwa
pamoja nawe ng'ambo ya Mto Yordani, yule
uliyeshuhudia habari zake, sasa anabatiza
na kila mtu anamwendea!"

27 [j]Yohana akawajibu, "Hakuna mtu
yeyote awezaye kupata kitu chochote
isipokuwa kile tu alichopewa kutoka
mbinguni. 28 [k]Ninyi wenyewe ni mashahidi
wangu kwamba nilisema, 'Mimi si Kristo,[l]
ila nimetumwa nimtangulie.' 29 [m]Bibi arusi
ni wa bwana arusi. Lakini rafiki yake
bwana arusi anayesimama karibu naye na
kusikiliza kutoka kwake, hufurahi sana
aisikiapo sauti ya bwana arusi. Kwa sababu
hii furaha yangu imekamilika. 30 [n]Yeye hana
budi kuwa mkuu zaidi na mimi nizidi kuwa
mdogo."

*Yeye Aliyetoka Mbinguni*

31 [o]"Yeye ajaye kutoka juu yu juu ya
yote, yeye aliye wa duniani ni wa dunia,
naye huzungumza mambo ya duniani.
Yeye aliyekuja kutoka mbinguni, yu
juu ya yote. 32 [p]Yeye hushuhudia yale
aliyoyaona na kuyasikia, lakini hakuna
yeyote anayekubali ushuhuda wake.
33 [q]Lakini yeyote anayekubali huo ushuhuda
anathibitisha kwamba, Mungu ni kweli.
34 [r]Yeye aliyetumwa na Mungu husema
maneno ya Mungu, kwa kuwa Mungu
humtoa Roho pasipo kipimo. 35 [s]Baba
anampenda Mwana, naye ametia vitu vyote
mikononi mwake. 36 [t]Yeyote anayemwamini
Mwana ana uzima wa milele, lakini yeye
asiyemwamini Mwana hatauona uzima, bali
ghadhabu ya Mungu itakuwa juu yake."

*Yesu Azungumza Na Mwanamke Msamaria*

4 [u]Mafarisayo wakasikia kwamba Yesu
alikuwa anapata na kubatiza wanafunzi
wengi zaidi kuliko Yohana, 2 [v]ingawa
kwa kweli si Yesu mwenyewe aliyekuwa

---

[a]**3:17** Yn 17:8, 21; 20:21; Isa 53:11; Rum 11:14
[b]**3:18** Yn 5:24; 1:18; 1Yn 4:9
[c]**3:19** Yn 1:4; 8:12
[d]**3:20** Efe 5:11-13
[e]**3:22** Yn 4:2
[f]**3:23** 1Sam 9:4; Mt 3:6
[g]**3:24** Mt 4:12; 14:3
[h]**3:25** Yn 2:6
[i]**3:26** Mt 23:7; Yn 1:7
[j]**3:27** Ebr 5:4; 1Kor 4:7; Yak 1:17
[k]**3:28** Yn 1:20-23; 3:9; Mt 9:15; Flp 2:2; 2Yn 12
[l]28 *Kristo* maana yake ni *Masiya*, yaani *Aliyetiwa mafuta.*
[m]**3:29** Mt 22:2; 2Kor 11:2; Efe 5:25, 27; Ufu 21:9; Wim 5:1
[n]**3:30** 2Sam 3:1
[o]**3:31** Yn 8:23; 1Yn 4:5
[p]**3:32** Yn 8:26; 15:15
[q]**3:33** Rum 3:4; 1Yn 5:10
[r]**3:34** Isa 42:1; Mt 12:18
[s]**3:35** Mt 28:18; Yn 17:2
[t]**3:36** Yn 5:24; 6:47
[u]**4:1** Yn 3:22-26
[v]**4:2** 1Kor 1:17

akibatiza, ila ni wanafunzi wake. 3 [a]Bwana
alipojua mambo haya, aliondoka Uyahudi
akarudi tena Galilaya.
4 [b]Wakati huo ilimlazimu apitie Samaria.
5 [c]Akafika kwenye mji mmoja wa Samaria
uitwao Sikari, karibu na lile shamba ambalo
Yakobo alimpa mwanawe Yosefu. 6 Huko
ndiko kulikokuwa na kile kisima cha
Yakobo. Naye Yesu alikuwa amechoka kwa
kuwa alikuwa ametoka safarini. Akaketi
karibu na hicho kisima. Ilikuwa yapata saa
sita mchana.
7 [d]Mwanamke mmoja Msamaria akaja
kuteka maji, Yesu akamwambia, “Naomba
maji ninywe.” 8 [e](Wakati huo wanafunzi
wake walikuwa wamekwenda mjini
kununua chakula.)
9 [f]Yule mwanamke Msamaria akamjibu,
“Wewe ni Myahudi na mimi ni Msamaria.
Yawezekanaje uniombe nikupe maji
ya kunywa?” (Wayahudi walikuwa
hawashirikiani kabisa na Wasamaria.)
10 [g]Yesu akajibu akamwambia, “Kama
ungelijua karama ya Mungu, naye ni nani
anayekuambia, Nipe maji ninywe, wewe
ungelimwomba yeye, naye angelikupa maji
yaliyo hai.”
11 Yule mwanamke akamjibu, “Bwana,
wewe huna chombo cha kutekea maji na
kisima hiki ni kirefu. Hayo maji ya uzima
utayapata wapi? 12 [h]Kwani wewe ni mkuu
kuliko baba yetu Yakobo ambaye alitupatia
kisima hiki, ambacho yeye pamoja na
watoto wake na mifugo yake walikitumia?”
13 [i]Yesu akamjibu, “Kila mtu anayekunywa
maji ya kisima hiki ataona kiu tena.
14 [j]Lakini yeyote anywaye maji nitakayompa
hataona kiu kamwe. Maji nitakayompa
yatakuwa ndani yake chemchemi ya maji,
yakibubujika uzima wa milele.”
15 [k]Yule mwanamke akamwambia,
“Bwana, tafadhali nipe maji hayo ili
nisipate kiu tena na wala nisije tena hapa
kuteka maji!”
16 Yesu akamjibu, “Nenda ukamwite
mumeo, uje naye hapa.”
17 Yule mwanamke akajibu, “Sina mume.”
Yesu akamwambia, “Umesema
kweli kuwa huna mume. 18 Kwa maana
umeshakuwa na wanaume watano na
mwanaume unayeishi naye sasa si mume
wako! Umesema ukweli.”
19 [l]Yule mwanamke akasema, “Bwana,
naona bila shaka wewe ni nabii. 20 [m]Baba
zetu waliabudu kwenye mlima huu, lakini
ninyi Wayahudi mnasema ni lazima
tukaabudu huko Yerusalemu.”
21 [n]Yesu akamjibu, “Mwanamke, niamini,
wakati unakuja ambapo hamtamwabudu
Baba katika mlima huu, wala huko
Yerusalemu. 22 [o]Ninyi Wasamaria mnaabudu
msichokijua. Sisi Wayahudi tunamwabudu
Mungu tunayemjua kwa sababu wokovu
unatoka kwa Wayahudi. 23 [p]Lakini saa yaja,
tena ipo, ambapo wale waabuduo halisi,
watamwabudu Baba katika roho na kweli.
Watu wanaoabudu namna hii, ndio Baba
anawatafuta. 24 [q]Mungu ni Roho na wote
wanaomwabudu imewapasa kumwabudu
katika roho na kweli.”
25 [r]Yule mwanamke akamwambia,
“Ninafahamu kwamba Masiya (aitwaye
Kristo) anakuja. Yeye akija, atatueleza
mambo yote.”
26 [s]Yesu akamwambia, “Mimi
ninayezungumza nawe, ndiye.”
27 [t]Wakati huo wanafunzi wake wakarudi,
wakashangaa sana kumwona akizungumza
na mwanamke. Lakini hakuna aliyemuuliza,

---

[a]**4:3** Yn 3:22
[b]**4:4** Lk 9:52
[c]**4:5** Mwa 48:22; Yos 24:32
[d]**4:7** Mwa 24:17; 1Fal 17:10
[e]**4:8** Yn 4:5, 30
[f]**4:9** Mt 10:5; Lk 9:52-53
[g]**4:10** Isa 55:1; Ufu 21:6
[h]**4:12** Yn 4:6; 8:53
[i]**4:13** Yn 6:58
[j]**4:14** Yn 6:35; Isa 12:3; Yn 7:38; Mt 25:46
[k]**4:15** Yn 6:34
[l]**4:19** Mt 21:11
[m]**4:20** Kum 11:29; Yos 8:33; Lk 9:53; 4:21; 4:20; Yn 5:28; 16:2; 1Tim 2:8
[n]**4:21** Yn 5:28; 16:2; Mal 1:11; 1Tim 2:8
[o]**4:22** 2Fal 17:28-41; Isa 2:3; Rum 9:4-5
[p]**4:23** Yn 5:25; 16:32; Flp 3:3
[q]**4:24** Flp 3:3
[r]**4:25** Mt 1:16; Yn 1:41
[s]**4:26** Yn 8:24; 9:35-37
[t]**4:27** Yn 4:8

“Unataka nini kwake?” Au “Kwa nini
unazungumza naye?”
28 Yule mwanamke akaacha mtungi wake,
akarudi mjini akawaambia watu, 29 [a]“Njooni
mkamwone mtu aliyeniambia kila kitu
nilichotenda! Je, yawezekana huyu ndiye
Kristo?”[b] 30 Basi wakamiminika watu kutoka
mjini wakamwendea Yesu.
31 [c]Wakati huo wanafunzi wake walikuwa
wakimsihi, “Rabi, kula angalau chochote.”
32 [d]Lakini yeye akawajibu, “Mimi ninacho
chakula ambacho ninyi hamkifahamu.”
33 Basi wanafunzi wakaanza kuulizana,
“Kuna mtu ambaye amemletea chakula?”
34 [e]Lakini Yesu akawajibu, “Chakula changu
ni kufanya mapenzi ya Mungu ambaye
amenituma na kuikamilisha kazi yake. 35 [f]Je,
ninyi hamsemi, ‘Bado miezi minne tuvune?’
Inueni macho yenu myaangalie mashamba
jinsi mazao yalivyo tayari kuvunwa!
36 [g]Mvunaji tayari anapokea mshahara
wake, naye anakusanya mazao kwa ajili
ya uzima wa milele. Ili yeye apandaye na
yeye avunaye wafurahi pamoja. 37 [h]Hivyo
kule kusema, ‘Mmoja hupanda na mwingine
huvuna,’ ni kweli kabisa. 38 Niliwatuma
mkavune mazao ambayo hamkupanda,
wengine walifanya kazi ngumu, nanyi
mmevuna faida ya taabu yao.”

*Wasamaria Wengi Waamini*

39 [i]Wasamaria wengi katika mji
ule wakamwamini Yesu kwa sababu
ya ushuhuda wa yule mwanamke
alipowaambia kwamba, “Ameniambia kila
kitu nilichotenda.” 40 Hivyo wale Wasamaria
walipomjia, wakamsihi akae kwao. Naye
akakaa huko siku mbili. 41 Kwa sababu ya
neno lake, watu wengi wakaamini.
42 [j]Wakamwambia yule mwanamke,
“Sasa tunaamini, wala si kwa sababu ya
maneno yako tu, bali kwa kuwa tumemsikia
sisi wenyewe. Tumejua hakika kweli ya
kwamba huyu ndiye Kristo, Mwokozi wa
ulimwengu.”

*Yesu Amponya Mwana Wa Afisa*

43 Baada ya zile siku mbili, Yesu aliondoka
kwenda Galilaya. 44 [k](Basi Yesu mwenyewe
alikuwa amesema kwamba nabii hapati
heshima katika nchi yake mwenyewe.)
45 [l]Alipofika Galilaya, Wagalilaya
walimkaribisha, kwani walikuwa wameona
yale aliyoyatenda huko Yerusalemu wakati
wa Sikukuu ya Pasaka. Kwa maana wao
pia walikuwa wamehudhuria hiyo Sikukuu.
46 [m]Hivyo Yesu akaja tena mpaka Kana ya
Galilaya, kule alikokuwa amebadili maji
kuwa divai. Huko kulikuwepo na afisa
mmoja wa mfalme, ambaye mwanawe
alikuwa mgonjwa huko Kapernaumu.
47 [n]Huyo mtu aliposikia kwamba Yesu
alikuwa amewasili Galilaya kutoka
Uyahudi, alimwendea na kumwomba ili aje
kumponya mwanawe, aliyekuwa mgonjwa
karibu ya kufa.
48 [o]Yesu akamwambia, “Ninyi watu
msipoona ishara na miujiza kamwe
hamtaamini.”
49 Yule afisa wa mfalme akamwambia,
“Bwana, tafadhali shuka kabla mwanangu
hajafa.”
50 Yesu akamjibu, “Enenda zako, mwanao
yu hai.”
Yule afisa akaamini yale maneno Yesu
aliyomwambia, akaondoka akaenda zake.
51 Alipokuwa bado yuko njiani, akakutana
na watumishi wake wakamwambia kwamba
mwanawe yu mzima. 52 Akawauliza
saa ambayo alianza kupata nafuu.
Wakamwambia, “Jana yapata saa saba,
homa ilimwacha.”

---

[a]**4:29** Mt 12:23; Yn 7:26, 31
[b]29 *Kristo* maana yake ni *Masiya*, yaani *Aliyetiwa mafuta.*
[c]**4:31** Mt 23:7
[d]**4:32** Ay 23:12; Mt 4:4
[e]**4:34** Mt 26:39; Yn 17:4; 19:30
[f]**4:35** Mt 9:37; Lk 10:2
[g]**4:36** Rum 1:13; Mt 25:46
[h]**4:37** Ay 31:8; Mik 6:15
[i]**4:39** Yn 4:29
[j]**4:42** Lk 2:11; 1Yn 4:14
[k]**4:44** Mt 13:57; Lk 4:24
[l]**4:45** Yn 2:23
[m]**4:46** Yn 21:1-11
[n]**4:47** Yn 4:3, 54; Lk 7:2
[o]**4:48** Dan 4:2-3; Ebr 2:4

53 [a]Ndipo baba wa huyo mtoto
akakumbuka kuwa huo ndio wakati ambapo
Yesu alikuwa amemwambia, “Mwanao yu
hai.” Kwa hiyo yeye pamoja na wote wa
nyumbani mwake wakamwamini Yesu.
54 [b]Hii ilikuwa ishara ya pili ambayo Yesu
alifanya aliporudi Galilaya kutoka Uyahudi.

*Yesu Amponya Mtu Kwenye Bwawa La Bethzatha*

5 [c]Baada ya haya, kulikuwa na Sikukuu ya
Wayahudi, naye Yesu akapanda kwenda
Yerusalemu. 2 [d]Huko Yerusalemu, karibu
na mlango uitwao Mlango wa Kondoo,
palikuwa na bwawa moja lililoitwa kwa
Kiebrania Bethzatha,[e] ambalo lilikuwa
limezungukwa na kumbi tano. 3 Hapa
palikuwa na idadi kubwa ya wasiojiweza,
yaani, vipofu, viwete, na waliopooza
[wakingojea maji yatibuliwe. 4 Kwa maana
malaika alikuwa akishuka wakati fulani,
akayatibua maji. Yule aliyekuwa wa kwanza
kuingia ndani baada ya maji kutibuliwa
alipona ugonjwa wowote aliokuwa nao].
5 Mtu mmoja alikuwako huko ambaye
alikuwa ameugua kwa miaka thelathini na
minane. 6 Yesu alipomwona akiwa amelala
hapo, naye akijua kuwa amekuwa hapo kwa
muda mrefu, akamwambia, “Je, wataka
kuponywa?”
7 Yule mgonjwa akamjibu, “Bwana,
mimi sina mtu wa kuniingiza bwawani
maji yanapotibuliwa. Nami ninapotaka
kutumbukia bwawani, mtu mwingine
huingia kabla yangu.”
8 [f]Yesu akamwambia, “Inuka! Chukua
mkeka wako na uende.” 9 [g]Mara yule mtu
akapona, akachukua mkeka wake, akaanza
kutembea.
Basi siku hiyo ilikuwa siku ya Sabato.
10 [h]Kwa hiyo Wayahudi wakamwambia yule
mtu aliyeponywa, “Leo ni Sabato, si halali
wewe kubeba mkeka wako.”
11 Yeye akawajibu, “Yule mtu
aliyeniponya aliniambia, ‘Chukua mkeka
wako na uende.’ ”
12 [i]Wakamuuliza, “Ni mtu gani huyo
aliyekuambia uchukue mkeka wako
uende?”
13 Basi yule mtu aliyeponywa hakufahamu
ni nani aliyemponya, kwa sababu Yesu
alikuwa amejiondoa katika ule umati wa
watu uliokuwa hapo.
14 [j]Baadaye Yesu akamkuta yule
mtu aliyemponya ndani ya Hekalu na
kumwambia, “Tazama umeponywa,
usitende dhambi tena. La sivyo, lisije
likakupata jambo baya zaidi.” 15 [k]Yule mtu
akaenda, akawaambia wale Wayahudi
kuwa ni Yesu aliyemponya.

*Uzima Kupitia Mwana*

16 [l]Kwa hiyo Wayahudi wakaanza
kumsumbua Yesu, kwa sababu alikuwa
anafanya mambo kama hayo siku ya
Sabato. 17 [m]Yesu akawajibu, “Baba yangu
anafanya kazi yake daima hata siku hii ya
leo, nami pia ninafanya kazi.” 18 [n]Maneno
haya yaliwaudhi sana viongozi wa
Wayahudi. Wakajaribu kila njia wapate
jinsi ya kumuua, kwani si kwamba alivunja
Sabato tu, bali alikuwa akimwita Mungu
Baba yake, hivyo kujifanya sawa na Mungu.

*Mamlaka Ya Mwana Wa Mungu*

19 [o]Yesu akawaambia, “Amin, amin
nawaambia, Mwana hawezi kufanya jambo
lolote peke yake, yeye aweza tu kufanya
lile analomwona Baba yake akifanya, kwa

[a]**4:53** Mdo 11:14
[b]**4:54** Yn 4:8; 2:11
[c]**5:1** Law 23:2; Kum 16:1; Yn 2:13
[d]**5:2** Neh 3:1; 12:39; Mdo 21:40; 26:14
[e]2 Bethzatha ni neno la Kiebrania ambalo maana yake ni Nyumba ya mizeituni; mahali pengine limetajwa kama Bethesda kwa Kiaramu, yaani Nyumba ya huruma, na pengine kama Bethsaida, yaani Nyumba ya uvuvi.
[f]**5:8** Mk 2:11; Lk 5:24
[g]**5:9** Mt 12:1-14; Yn 9:14
[h]**5:10** Yer 17:21; Mt 12:2
[i]**5:12** Lk 5:21
[j]**5:14** Mk 2:5; Yn 8:11; 8:11
[k]**5:15** Yn 1:19
[l]**5:16** Mt 12:14
[m]**5:17** Yn 9:4; 14:10
[n]**5:18** Mt 12:14; Yn 10:30-33; 19:7
[o]**5:19** Yn 8:28; 14:24

maana lolote afanyalo Baba, Mwana pia
hufanya vivyo hivyo. 20 [a]Baba ampenda
Mwana na kumwonyesha yale ambayo
yeye Baba mwenyewe anayafanya, naye
atamwonyesha kazi kuu kuliko hizi ili
mpate kushangaa. 21 [b]Hakika kama vile
Baba awafufuavyo wafu na kuwapa uzima,
vivyo hivyo Mwana huwapa uzima wale
anaopenda. 22 [c]Wala Baba hamhukumu
mtu yeyote, lakini hukumu yote amempa
Mwana, 23 [d]ili wote wamheshimu Mwana
kama vile wanavyomheshimu Baba. Yeyote
asiyemheshimu Mwana, hamheshimu Baba
aliyemtuma.

24 [e]“Amin, amin nawaambia, yeyote
anayesikia maneno yangu na kumwamini
yeye aliyenituma, anao uzima wa milele,
naye hatahukumiwa, bali amepita kutoka
mautini, na kuingia uzimani. 25 [f]Amin, amin
nawaambia, saa yaja, nayo saa ipo, wafu
watakapoisikia sauti ya Mwana wa Mungu,
nao watakaoisikia watakuwa hai. 26 [g]Kama
vile Baba alivyo na uzima ndani yake, vivyo
hivyo amempa Mwana kuwa na uzima
ndani yake. 27 [h]Naye amempa Mwanawe
mamlaka ya kuhukumu kwa kuwa yeye ni
Mwana wa Adamu.

28 [i]“Msishangae kusikia haya, kwa maana
saa inakuja ambapo wale walio makaburini
wataisikia sauti yake. 29 [j]Nao watatoka
nje, wale waliotenda mema watafufuka
wapate uzima na wale waliotenda maovu,
watafufuka wahukumiwe.

### *Shuhuda Kuhusu Yesu*

30 [k]“Mimi siwezi kufanya jambo
lolote peke yangu. Ninavyosikia ndivyo
ninavyohukumu, nayo hukumu yangu ni
ya haki kwa kuwa sitafuti kufanya mapenzi
yangu mwenyewe, bali mapenzi yake yeye
aliyenituma.

31 [l]“Kama ningejishuhudia mimi
mwenyewe, ushuhuda wangu si kweli.
32 [m]Lakini yuko mwingine anishuhudiaye
na ninajua kwamba ushuhuda wake ni wa
kweli.

33 [n]“Mlituma wajumbe kwa Yohana, naye
akashuhudia juu ya kweli. 34 [o]Si kwamba
naukubali ushuhuda wa mwanadamu,
la, bali ninalitaja hili kusudi ninyi mpate
kuokolewa. 35 [p]Yohana alikuwa taa
iliyowaka na kutoa nuru, nanyi kwa muda
mlichagua kuifurahia nuru yake.

36 [q]“Lakini ninao ushuhuda mkuu zaidi
kuliko wa Yohana. Kazi zile nizifanyazo,
zinashuhudia juu yangu, zile ambazo Baba
amenituma nizikamilishe, naam, ishara
hizi ninazofanya, zinashuhudia kuwa Baba
ndiye alinituma. 37 [r]Naye Baba mwenyewe
ameshuhudia juu yangu. Hamjapata
kamwe kuisikia sauti yake wala kuona
umbo lake, 38 [s]wala hamna neno lake ndani
yenu, kwa sababu hamkumwamini yeye
aliyetumwa naye. 39 [t]Ninyi mnachunguza
Maandiko mkidhani ya kuwa ndani yake
mna uzima wa milele, maandiko haya
ndiyo yanayonishuhudia Mimi. 40 [u]Lakini
mnakataa kuja kwangu ili mpate uzima.

41 [v]“Mimi sitafuti kutukuzwa na
wanadamu. 42 Lakini ninajua kwamba
hamna upendo wa Mungu mioyoni mwenu.
43 Mimi nimekuja kwa jina la Baba yangu,
nanyi hamnipokei, lakini mtu mwingine
akija kwa jina lake mwenyewe, mtampokea.
44 [w]Ninyi mwawezaje kuamini ikiwa
mnapeana utukufu ninyi kwa ninyi, lakini
hamna bidii kupata utukufu utokao kwa
Mungu?

[a]**5:20** Yn 3:35; 14:12
[b]**5:21** 2Kor 1:9; Ebr 11:19; Yn 11:25
[c]**5:22** Amu 11:27; Mdo 10:42
[d]**5:23** Lk 10:16; 1Yn 2:23
[e]**5:24** Yn 3:18; 1Yn 3:14
[f]**5:25** Yn 16:32; 8:43-47
[g]**5:26** Yn 12:14
[h]**5:27** Mdo 10:42; 17:31
[i]**5:28** Yn 16:2
[j]**5:29** Dan 12:2; Mt 25:46
[k]**5:30** Isa 28:6; Mt 26:39; Yn 4:34
[l]**5:31** Yn 8:14
[m]**5:32** Yn 5:37; 8:18
[n]**5:33** Yn 1:7
[o]**5:34** 1Yn 5:9
[p]**5:35** Dan 12:3
[q]**5:36** 1Yn 5:9; Yn 14:11; 15:24; 3:17; 10:25
[r]**5:37** Yn 8:18; Kum 4:12; 1Tim 1:17
[s]**5:38** 1Yn 1:10; 2:4; Isa 26:10; Yn 3:17
[t]**5:39** Rum 2:17-18; Lk 24:27, 44; Mdo 13:27
[u]**5:40** Yn 6:44
[v]**5:41** Yn 5:44; 5:34; 1The 2:6
[w]**5:44** Rum 2:29

45 [a]“Lakini msidhani kuwa mimi
nitawashtaki mbele za Baba, mshtaki
wenu ni Mose, ambaye mmemwekea
tumaini lenu. 46 [b]Kama mngelimwamini
Mose, mngeliniamini na mimi kwa maana
aliandika habari zangu. 47 [c]Lakini ikiwa
hamwamini aliyoandika Mose, mtaaminije
ninayoyasema?”

*Yesu Alisha Wanaume 5,000*

**(Mathayo 14:13-21; Marko 6:30-44; Luka 9:10-17)**

6 [d]Baada ya haya, Yesu alikwenda ng’ambo
ya Bahari ya Galilaya, ambayo pia
huitwa Bahari ya Tiberia. 2 [e]Umati mkubwa
wa watu uliendelea kumfuata, kwa sababu
waliona ishara nyingi za miujiza alizofanya
kwa wagonjwa. 3 [f]Kisha Yesu akapanda
mlimani akaketi huko pamoja na wanafunzi
wake. 4 [g]Pasaka ya Wayahudi ilikuwa
imekaribia.

5 [h]Yesu alipotazama na kuuona ule umati
mkubwa wa watu ukimjia, akamwambia
Filipo, “Tutanunua wapi mikate ili watu
hawa wale?” 6 Aliuliza swali hili kumpima,
kwa maana alishajua la kufanya.

7 [i]Filipo akamjibu, “Hata fedha kiasi cha
dinari mia mbili,[j] hazitoshi kununua mikate
ya kuwapa watu hawa ili kila mtu apate
kidogo.”

8 [k]Mmoja wa wanafunzi wake aitwaye
Andrea, ndugu yake Simoni Petro,
akamwambia, 9 [l]“Hapa kuna mvulana
mmoja mwenye mikate mitano ya shayiri
na samaki wawili wadogo. Lakini hivi
vitatosha nini kwa umati huu wote?”

10 Yesu akasema, “Waketisheni watu
chini.” Palikuwa na majani mengi katika
eneo lile, nao watu wakaketi. Palikuwa na
wanaume wapatao 5,000. 11 [m]Ndipo Yesu
akachukua ile mikate, akamshukuru Mungu
na kuwagawia wale watu waliokuwa
wameketi. Akafanya vivyo hivyo na wale
samaki. Kila mtu akapata kadiri alivyotaka.

12 Watu wote walipokwisha kula na
kushiba, akawaambia wanafunzi wake,
“Kusanyeni vipande vilivyobaki vya ile
mikate, kisipotee chochote.” 13 Hivyo
wakavikusanya, wakajaza vikapu kumi na
viwili kwa vipande vya ile mikate mitano
ya shayiri na samaki wale wawili wadogo
vilivyobakishwa na waliokula.

14 [n]Baada ya watu kuona muujiza ule Yesu
aliofanya, walianza kusema, “Hakika huyu
ndiye Nabii ajaye ulimwenguni!” 15 [o]Yesu
akijua kwamba walitaka kuja kumfanya
awe mfalme wao, kwa nguvu, akajitenga
nao akaenda milimani peke yake.

*Yesu Atembea Juu Ya Maji*

**(Mathayo 14:22-33; Marko 6:45-52)**

16 [p]Ilipofika jioni, wanafunzi wake
waliteremka kwenda baharini. 17 Wakaingia
kwenye mashua, wakaanza kuvuka bahari
kwenda Kapernaumu. Wakati huu kulikuwa
tayari giza na Yesu alikuwa hajajumuika
nao. 18 Bahari ikachafuka kwa sababu upepo
mkali ulikuwa unavuma. 19 [q]Wanafunzi
walipokuwa wamekwenda mwendo wa
karibu maili tatu au nne,[r] walimwona
Yesu akitembea juu ya maji akikaribia
mashua, nao wakaogopa sana. 20 [s]Lakini
Yesu akawaambia, “Ni mimi. Msiogope.”
21 Ndipo wakamkaribisha kwa furaha
ndani ya mashua, na mara wakafika ufuoni
walikokuwa wakienda.

---

[a] **5:45** Yn 9:28; Rum 2:17
[b] **5:46** Mwa 3:15; Lk 24:27, 44
[c] **5:47** Lk 16:29-31
[d] **6:1** Mt 14:15; Mk 6:35; Lk 9:10, 12
[e] **6:2** Yn 2:11-13
[f] **6:3** Yn 6:15
[g] **6:4** Yn 11:55
[h] **6:5** Yn 1:43
[i] **6:7** Hes 11:21, 22
[j] 7 Dinari 200 ni sawa na mshahara wa kibarua wa siku 200; mshahara wa kibarua ulikuwa dinari moja kwa siku.
[k] **6:8** Yn 1:40
[l] **6:9** 2Fal 4:43
[m] **6:11** Mt 14:19
[n] **6:14** Yn 2:11; Kum 18:15-18; Mt 21:11
[o] **6:15** Yn 18:36; Mt 14:23; Mk 6:46
[p] **6:16** Mt 14:22-33; Mk 6:45-52
[q] **6:19** Ay 9:8
[r] 19 Maili tatu au nne ni kama kilomita 5 au 6.
[s] **6:20** Mt 14:27

*Watu Wanamtafuta Yesu*

22 [a]Siku iliyofuata, wale watu waliokuwa
wamebaki ng'ambo waliona kwamba
palikuwepo na mashua moja tu na kwamba
Yesu hakuwa ameondoka pamoja na
wanafunzi wake, ila walikuwa wameondoka
peke yao. 23 [b]Lakini zikaja mashua nyingine
kutoka Tiberia zikafika karibu na mahali
pale walipokula mikate baada ya Bwana
kumshukuru Mungu. 24 Mara wale watu
wakatambua kwamba Yesu hakuwepo hapo,
wala wanafunzi wake. Wakaingia kwenye
mashua hizo, wakaenda Kapernaumu ili
kumtafuta Yesu.

*Yesu Ni Mkate Wa Uzima*

25 [c]Walipomkuta Yesu ng'ambo ya bahari
wakamuuliza, "Rabi, umefika lini huku?"
26 [d]Yesu akawajibu, "Amin, amin
nawaambia, ninyi hamnitafuti kwa
kuwa mliona ishara na miujiza, bali kwa
sababu mlikula ile mikate mkashiba.
27 [e]Msishughulikie chakula kiharibikacho,
bali chakula kidumucho hata uzima
wa milele, ambacho Mwana wa Adamu
atawapa. Yeye ndiye ambaye Mungu Baba
amemtia muhuri."
28 Ndipo wakamuuliza, "Tufanye nini ili
tupate kuitenda kazi ya Mungu?"
29 [f]Yesu akawajibu, "Kazi ya Mungu ndiyo
hii: Mwamininі yeye aliyetumwa naye."
30 [g]Hivyo wakamuuliza, "Utafanya ishara
gani ya muujiza, ili tuione tukuamini?
Utafanya jambo gani? 31 [h]Baba zetu walikula
mana jangwani, kama ilivyoandikwa,
'Aliwapa mikate kutoka mbinguni ili wale.' "
32 [i]Yesu akawaambia, "Amin, amin
nawaambia, si Mose aliyewapa mikate
kutoka mbinguni, bali Baba yangu ndiye
anawapa mkate wa kweli kutoka mbinguni.
33 [j]Kwa maana mkate wa Mungu ni yule
ashukaye kutoka mbinguni na kuupa
ulimwengu uzima."
34 [k]Wakamwambia, "Bwana, kuanzia sasa
tupatie huo mkate siku zote."
35 [l]Yesu akawaambia, "Mimi ndimi mkate
wa uzima. Yeye ajaye kwangu, hataona njaa
kamwe na yeye aniaminiye, hataona kiu
kamwe. 36 [m]Lakini kama nilivyowaambia,
mmeniona lakini bado hamwamini. 37 [n]Wale
wote anipao Baba watakuja kwangu na
yeyote ajaye kwangu, sitamfukuzia nje
kamwe. 38 [o]Kwa kuwa nimeshuka kutoka
mbinguni si ili kufanya mapenzi yangu, bali
mapenzi yake yeye aliyenituma. 39 [p]Haya
ndiyo mapenzi yake yeye aliyenituma,
kwamba, nisimpoteze hata mmoja wa wale
alionipa, bali niwafufue siku ya mwisho.
40 [q]Kwa maana mapenzi ya Baba yangu ni
kwamba kila mmoja amtazamaye, Mwana
na kumwamini awe na uzima wa milele,
nami nitawafufua siku ya mwisho."
41 Wayahudi wakaanza kunung'unika
kwa kuwa alisema, "Mimi ndimi mkate
ulioshuka kutoka mbinguni." 42 [r]Wakasema,
"Huyu si Yesu, mwana wa Yosefu, ambaye
baba yake na mama yake tunawajua?
Anawezaje basi sasa kusema, 'Nimeshuka
kutoka mbinguni'?"
43 Hivyo Yesu akawaambia, "Acheni
kunung'unikiana ninyi kwa ninyi. 44 Hakuna
mtu awezaye kuja kwangu kama asipovutwa
na Baba aliyenituma, nami nitamfufua siku
ya mwisho. 45 [s]Imeandikwa katika Manabii,
'Wote watafundishwa na Mungu.' Yeyote
amsikilizaye Baba na kujifunza kutoka
kwake, huyo huja kwangu. 46 [t]Hakuna
mtu yeyote aliyemwona Baba isipokuwa
yeye atokaye kwa Mungu, yeye ndiye peke

[a]**6:22** Yn 6:2; 15:21
[b]**6:23** Yn 6:1, 11
[c]**6:25** Mt 23:7
[d]**6:26** Yn 2:11
[e]**6:27** Mt 25:46; Yn 4:14; Mt 8:20; 2Tim 2:19; Ufu 7:3
[f]**6:29** 1Yn 3:23; 3:17
[g]**6:30** Yn 2:11; Mt 12:38
[h]**6:31** Hes 11:7-9; Neh 9:15; Za 105:40
[i]**6:32** Yn 6:49
[j]**6:33** Yn 3:13, 31
[k]**6:34** Yn 4:15
[l]**6:35** Yn 4:14; 6:48; 7:37
[m]**6:36** Yn 6:26, 29
[n]**6:37** Yn 17:2-6, 9, 24
[o]**6:38** Yn 3:17; 4:34
[p]**6:39** Isa 27:3; Yn 18:9
[q]**6:40** Mt 25:26
[r]**6:42** Lk 4:22; Yn 7:27, 28
[s]**6:45** Isa 54:13; 1Kor 2:13
[t]**6:46** Yn 1:18; 7:29

yake aliyemwona Baba. 47 [a]Amin, amin
nawaambia, yeye anayeamini anao uzima
wa milele. 48 [b]Mimi ni mkate wa uzima.
49 [c]Baba zenu walikula mana jangwani,
lakini wakafa. 50 [d]Lakini hapa kuna mkate
utokao mbinguni, ambao mtu yeyote akiula,
hatakufa. 51 [e]Mimi ni mkate wa uzima ule
uliotoka mbinguni. Mtu yeyote akiula
mkate huu, ataishi milele. Mkate huu ni
mwili wangu, ambao nitautoa kwa ajili ya
uzima wa ulimwengu."

52 [f]Ndipo Wayahudi wakaanza kuhojiana
vikali wao kwa wao wakisema, "Mtu huyu
awezaje kutupatia mwili wake tuule?"

53 [g]Hivyo Yesu akawaambia, "Amin, amin
nawaambia, msipoula mwili wa Mwana wa
Adamu na kuinywa damu yake, hamna
uzima ndani yenu. 54 [h]Mtu yeyote aulaye
mwili wangu na kunywa damu yangu,
anao uzima wa milele. Nami nitamfufua
siku ya mwisho. 55 Kwa maana mwili wangu
ni chakula cha kweli na damu yangu ni
kinywaji cha kweli. 56 [i]Yeyote alaye mwili
wangu na kunywa damu yangu, atakaa
ndani yangu nami nitakaa ndani yake.
57 [j]Kama vile Baba aliye hai alivyonituma
mimi, na kama nami ninavyoishi kwa
sababu ya Baba, hivyo anilaye mimi ataishi
kwa sababu yangu. 58 [k]Huu ndio mkate
ushukao kutoka mbinguni, si kama ule
mkate baba zenu waliokula nao wakafa.
Lakini yeye aulaye mkate huu ataishi
milele." 59 Yesu alisema maneno haya
alipokuwa akifundisha katika sinagogi huko
Kapernaumu.

*Wafuasi Wengi Wamwacha Yesu*

60 [l]Wengi wa wafuasi wake waliposikia
jambo hili wakasema, "Mafundisho haya
ni magumu. Ni nani awezaye kuyapokea?"

61 [m]Yesu alipojua kwamba wafuasi wake
wananung'unika kuhusu mafundisho yake,
akawaambia, "Je, jambo hili limewaudhi?
62 [n]Ingekuwaje basi kama mngemwona
Mwana wa Adamu akipaa kwenda zake
huko alipokuwa kwanza? 63 [o]Roho ndiye
atiaye uzima, mwili haufai kitu. Maneno
haya niliyowaambia ni Roho tena ni uzima.
64 [p]Lakini baadhi yenu hamwamini." Kwa
maana Yesu alifahamu tangu mwanzo wale
ambao hawangemwamini miongoni mwao
na yule ambaye angemsaliti. 65 [q]Akaendelea
kusema, "Hii ndiyo sababu niliwaambia
kwamba hakuna mtu awezaye kuja kwangu
isipokuwa amejaliwa na Baba yangu."

66 [r]Tangu wakati huo wafuasi wake wengi
wakarejea nyuma wakaacha kumfuata.

67 [s]Hivyo Yesu akawauliza wale
wanafunzi wake kumi na wawili, "Je, ninyi
pia mnataka kuondoka?"

68 [t]Simoni Petro akamjibu, "Bwana,
tuondoke twende kwa nani? Wewe unayo
maneno ya uzima wa milele. 69 [u]Tunaamini
na kujua kuwa wewe ndiwe Aliye Mtakatifu
wa Mungu."

70 [v]Ndipo Yesu akajibu, "Je, sikuwachagua
ninyi kumi na wawili? Lakini mmoja wenu
ni ibilisi." 71 [w](Hapa alikuwa anasema juu ya
Yuda, mwana wa Simoni Iskariote. Ingawa
alikuwa mmoja wa wale kumi na wawili,
ndiye ambaye baadaye angemsaliti Yesu.)

*Kutokuamini Kwa Ndugu Zake Yesu*

7 [x]Baada ya mambo haya, Yesu alikwenda
sehemu mbalimbali za Galilaya. Hakutaka
kwenda Uyahudi kwa sababu Wayahudi

---

[a]**6:47** Mt 25:46
[b]**6:48** Yn 6:35, 51
[c]**6:49** Yn 6:3, 58
[d]**6:50** Yn 6:33
[e]**6:51** Ebr 10:10
[f]**6:52** Yn 9:16; 10:19
[g]**6:53** Mt 26:26; 8:20; 26:28
[h]**6:54** Yn 6:39
[i]**6:56** 1Yn 2:24; 3:24
[j]**6:57** Yn 3:17
[k]**6:58** Yn 3:36; 5:24
[l]**6:60** Yn 6:66; 6:52
[m]**6:61** Mt 13:57
[n]**6:62** Mk 16:19; Yn 17:5
[o]**6:63** 2Kor 3:6
[p]**6:64** Yn 2:24-25
[q]**6:65** Mt 13:11
[r]**6:66** Yn 6:60
[s]**6:67** Mt 10:2
[t]**6:68** Mt 16:16
[u]**6:69** Mk 1:24; Lk 9:20
[v]**6:70** Yn 15:16-19; 13:27; 17:12
[w]**6:71** Mt 26:14; 10:4
[x]**7:1** Yn 1:19; 5:18; Mt 12:18

huko walitaka kumuua. 2 [a]Sikukuu ya
Vibanda ya Wayahudi ilikuwa imekaribia.
3 [b]Hivyo ndugu zake Yesu wakamwambia,
“Ondoka hapa uende Uyahudi ili wanafunzi
Wako wapate kuona miujiza unayofanya.
4 Mtu anayetaka kujulikana hafanyi mambo
yake kwa siri. Kama unafanya mambo haya,
jionyeshe kwa ulimwengu.” 5 [c]Hata ndugu
zake mwenyewe hawakumwamini.

6 [d]Yesu akawaambia, “Wakati wangu bado
haujawadia, lakini wakati wenu upo siku
zote. 7 [e]Ulimwengu hauwezi kuwachukia
ninyi, lakini unanichukia mimi kwa sababu
ninawashuhudia kwamba matendo yao ni
maovu. 8 [f]Ninyi nendeni kwenye Sikukuu,
lakini mimi sitahudhuria Sikukuu hii
kwa sababu wakati wangu haujawadia.”
9 Akiisha kusema hayo, akabaki Galilaya.

*Yesu Kwenye Sikukuu Ya Vibanda*

10 Lakini ndugu zake walipokwisha
kuondoka kwenda kwenye Sikukuu, yeye
pia alikwenda lakini kwa siri. 11 [g]Wayahudi
walikuwa wakimtafuta huko kwenye
Sikukuu na kuulizana, “Yuko wapi huyu
mtu?”

12 [h]Kulikuwa na minong’ono iliyoenea
kumhusu Yesu katika umati wa watu, wakati
wengine wakisema, “Ni mtu mwema.”

Wengine walikuwa wakisema, “La, yeye
anawadanganya watu.” 13 [i]Lakini hakuna
mtu yeyote aliyemsema waziwazi kumhusu
kwa sababu ya kuwaogopa Wayahudi.

*Yesu Afundisha Kwenye Sikukuu*

14 [j]Ilipokaribia katikati ya Sikukuu, Yesu
alipanda kwenda Hekaluni na kuanza
kufundisha. 15 [k]Wayahudi wakastaajabia
mafundisho yake wakasema, “Mtu huyu
amepataje kujua mambo haya bila
kufundishwa?”

16 [l]Ndipo Yesu akawajibu, “Mafundisho
yangu si yangu mwenyewe, bali yanatoka
kwake yeye aliyenituma. 17 [m]Mtu yeyote
akipenda kufanya mapenzi ya Mungu,
atajua kama mafundisho yangu yanatoka
kwa Mungu au ninasema kwa ajili yangu
mwenyewe. 18 [n]Wale wanenao kwa ajili
yao wenyewe hufanya hivyo kwa kutaka
utukufu wao wenyewe. Lakini yeye
atafutaye utukufu wa yule aliyemtuma ni
wa kweli, wala hakuna uongo ndani yake.
19 [o]Je, Mose hakuwapa ninyi sheria? Lakini
hakuna hata mmoja wenu anayeishika hiyo
sheria. Kwa nini mnataka kuniua?”

20 [p]Ule umati wa watu ukamjibu, “Wewe
una pepo mchafu! Ni nani anayetaka
kukuua?”

21 [q]Yesu akawajibu, “Nimefanya muujiza
mmoja na nyote mkastaajabu. 22 [r]Lakini kwa
kuwa Mose aliwaamuru tohara (ingawa
kwa kweli haikutoka kwa Mose bali kwa
baba zenu wakuu), mnamtahiri mtoto
hata siku ya Sabato. 23 [s]Ikiwa mtoto aweza
kutahiriwa siku ya Sabato kusudi sheria ya
Mose isivunjwe, kwa nini mnanikasirikia
kwa kumponya mtu mwili wake wote siku
ya Sabato? 24 [t]Acheni kuhukumu mambo
kwa jinsi mnavyoona tu, bali hukumuni
kwa haki.”

*Je, Yesu Ndiye Kristo?*

25 [u]Ndipo baadhi ya watu wa Yerusalemu
wakawa wanasema, “Tazameni, huyu si
yule mtu wanayetaka kumuua? 26 [v]Mbona
yuko hapa anazungumza hadharani na
wala hawamwambii neno lolote? Je,

---

[a]**7:2** Law 23:34; Kum 16:16
[b]**7:3** Mt 12:46
[c]**7:5** Za 69:8; Mk 3:21
[d]**7:6** Mt 26:18
[e]**7:7** Yn 3:19-20; 15:18-19
[f]**7:8** Yn 7:6; Mt 26:18; Yn 8:30
[g]**7:11** Yn 11:56
[h]**7:12** Yn 9:16; 10:19; Mt 21:46; Lk 7:16; Yn 6:14
[i]**7:13** Yn 19:38; 20:19
[j]**7:14** Mt 26:55
[k]**7:15** Mdo 26:24; Mt 13:54
[l]**7:16** Yn 3:11; 14:24
[m]**7:17** Za 25:14; Yn 8:23
[n]**7:18** Yn 5:41; 8:50-54
[o]**7:19** Kum 32:46; Mt 12:14
[p]**7:20** Mk 3:22; Yn 10:20
[q]**7:21** Yn 5:16
[r]**7:22** Law 12:3; Mwa 17:10-14
[s]**7:23** Yn 5:8
[t]**7:24** 1Sam 16:7; 2Nya 10:7; Yn 8:15
[u]**7:25** Yn 7:19
[v]**7:26** Yn 7:48; 4:29

inawezekana viongozi wanafahamu kuwa
huyu ndiye Kristo?[a] 27 [b]Tunafahamu huyu
mtu anakotoka, lakini Kristo atakapokuja,
hakuna yeyote atakayejua atokako."
28 [c]Ndipo Yesu, akaendelea kufundisha
Hekaluni, akisema, "Ninyi mnanifahamu
na kujua nitokako. Mimi sikuja kwa ajili
yangu mwenyewe, bali yeye aliyenituma
ni wa kweli na ninyi hammjui. 29 [d]Mimi
namjua kwa kuwa nimetoka kwake, naye
ndiye alinituma."
30 [e]Ndipo wakatafuta kumkamata,
lakini hakuna mtu yeyote aliyethubutu
kumshika kwa sababu saa yake ilikuwa
bado haijawadia. 31 [f]Nao watu wengi
wakamwamini, wakasema, "Je, Kristo
atakapokuja, atafanya miujiza mikuu zaidi
kuliko aliyoifanya mtu huyu?"

*Walinzi Wanatumwa Kumkamata Yesu*

32 Mafarisayo wakasikia watu
wakinong'ona mambo kama hayo kuhusu
Yesu, ndipo wao pamoja na viongozi wa
makuhani wakatuma walinzi wa Hekalu
waende kumkamata.
33 [g]Yesu akasema, "Mimi bado niko
pamoja nanyi kwa kitambo kidogo,
kisha nitarudi kwake yeye aliyenituma.
34 [h]Mtanitafuta lakini hamtaniona, nami
niliko ninyi hamwezi kuja."
35 [i]Wayahudi wakaulizana wao kwa
wao, "Huyu mtu anataka kwenda
wapi ambako hatuwezi kumfuata? Je,
anataka kwenda kwa Wayunani ambako
baadhi ya watu wetu wametawanyikia,
akawafundishe Wayunani? 36 [j]Yeye ana
maana gani anaposema, 'Mtanitafuta
lakini hamtaniona,' na, 'nami niliko ninyi
hamwezi kuja'?"

*Mito Ya Maji Ya Uzima*

37 [k]Siku ile ya mwisho ya Sikukuu, siku
ile kuu, wakati Yesu akiwa amesimama
huko, akapaza sauti yake akasema, "Kama
mtu yeyote anaona kiu na aje kwangu
anywe. 38 [l]Yeyote aniaminiye mimi, kama
Maandiko yasemavyo, vijito vya maji
ya uzima vitatiririka ndani mwake."
39 [m]Yesu aliposema haya alimaanisha Roho
Mtakatifu ambaye wote waliomwamini
wangempokea, kwani mpaka wakati huo,
Roho alikuwa hajatolewa, kwa kuwa Yesu
alikuwa bado hajatukuzwa.

*Mgawanyiko Miongoni Mwa Watu*

40 [n]Waliposikia maneno hayo, baadhi ya
watu miongoni mwa ule umati wakasema,
"Hakika huyu ndiye yule Nabii."
41 [o]Wengine wakasema, "Huyu ndiye
Kristo!"
Lakini wengine wakauliza, "Je, Kristo
kwao ni Galilaya? 42 [p]Je, Maandiko hayasemi
kwamba Kristo atakuja kutoka jamaa ya
Daudi na kutoka Bethlehemu, mji alioishi
Daudi?" 43 [q]Kwa hiyo watu wakagawanyika
kwa ajili ya Yesu. 44 [r]Baadhi yao walitaka
kumkamata, lakini hakuna aliyethubutu
kumgusa.

*Kutokuamini Kwa Viongozi Wa Wayahudi*

45 [s]Hatimaye wale walinzi wa Hekalu
wakarudi kwa viongozi wa makuhani na
Mafarisayo waliokuwa wamewatuma ili
kumkamata Yesu, wakaulizwa, "Mbona
hamkumkamata?"
46 [t]Wale walinzi wakajibu, "Kamwe
hajanena mtu yeyote kama yeye anenavyo."
47 [u]Mafarisayo wakajibu, "Je, nanyi pia

---

[a]26 *Kristo* maana yake ni *Masiya*, yaani *Aliyetiwa mafuta.*
[b]**7:27** Mt 13:55; Lk 4:22
[c]**7:28** Yn 8:14, 26, 42
[d]**7:29** Mt 11:27
[e]**7:30** Yn 10:39
[f]**7:31** Yn 11:45; 12:11, 42; 2:11
[g]**7:33** Yn 16:5, 10, 17, 28
[h]**7:34** Yn 8:21; 13:33
[i]**7:35** Yak 1:1; Mdo 17:4; 1Pet 1:1
[j]**7:36** Yn 7:34
[k]**7:37** Law 23:36; Isa 55:1; Ufu 22:17
[l]**7:38** Isa 58:1; Yn 4:10
[m]**7:39** Yoe 2:28; Mdo 2:17, 33; Yn 20:22; 12:23; 13:31-32
[n]**7:40** Mt 2:11; Yn 1:21
[o]**7:41** Yn 7:52; 1:21
[p]**7:42** Mt 1:1; Mik 5:2; Mt 2:5-6
[q]**7:43** Yn 9:16; 10:9
[r]**7:44** Yn 7:30
[s]**7:45** Yn 7:32
[t]**7:46** Mt 7:28
[u]**7:47** Yn 7:12

mmedanganyika? 48 [a]Je, kuna kiongozi
yeyote au mmoja wa Mafarisayo ambaye
amemwamini? 49 Lakini huu umati wa watu
wasiojua Sheria ya Mose, wamelaaniwa."
50 [b]Ndipo Nikodemo, yule aliyekuwa
amemwendea Yesu siku moja usiku, ambaye
alikuwa mmoja wao akauliza, 51 [c]"Je, sheria
zetu zinaturuhusu kumhukumu mtu kabla
ya kumsikiliza na kufahamu alilotenda?"
52 [d]Wakamjibu, "Je, wewe pia unatoka
Galilaya? Chunguza nawe utaona kwamba
hakuna nabii atokae Galilaya!" [ 53 Kisha
wakaondoka, kila mtu akarudi nyumbani
kwake.

*Mwanamke Aliyefumaniwa Akizini*

8 [e]Lakini Yesu akaenda katika Mlima wa
Mizeituni. 2 [f]Alfajiri na mapema Yesu akaja
tena Hekaluni, watu wote wakakusanyika,
akakaa akaanza kuwafundisha. 3 Walimu
wa sheria na Mafarisayo wakamleta
mwanamke mmoja aliyefumaniwa akizini.
Wakamsimamisha katikati ya umati
wa watu wote. 4 Wakamwambia Yesu,
"Mwalimu, huyu mwanamke amekutwa
akizini. 5 [g]Katika sheria, Mose alituamuru
kuwapiga kwa mawe wanawake wa namna
hii, mpaka wafe. Sasa wewe wasemaje?"
6 [h]Walimuuliza swali hili kama mtego ili
wapate sababu ya kumshtaki.
Lakini Yesu akainama akaanza kuandika
ardhini kwa kidole chake. 7 [i]Walipoendelea
kumuulizauliza akainuka, akawaambia,
"Kama kuna mtu yeyote miongoni mwenu
ambaye hana dhambi na awe wa kwanza
kumtupia jiwe." 8 Akainama tena na
kuandika ardhini.
9 [j]Waliposikia haya, wakaanza kuondoka
mmoja mmoja, wakianzia wazee, hadi Yesu
akabaki peke yake na yule mwanamke
akiwa amesimama mbele yake. 10 Yesu
akainuka na kumwambia, "Wako wapi wale
waliokuwa wanakuhukumu kuwa mwenye
hatia?"
11 [k]Yule mwanamke akajibu, "Hakuna
hata mmoja Bwana."
Yesu akamwambia, "Hata mimi
sikuhukumu. Nenda zako, kuanzia sasa
usitende dhambi tena."]

*Yesu Nuru Ya Ulimwengu*

12 [l]Kisha Yesu akasema nao tena
akawaambia, "Mimi ni nuru ya ulimwengu.
Mtu yeyote akinifuata hatatembea gizani
kamwe, bali atakuwa na nuru ya uzima."
13 [m]Mafarisayo wakamwambia, "Ushuhuda
wako haukubaliki kwa kuwa unajishuhudia
mwenyewe."
14 [n]Yesu akawajibu, "Hata kama
najishuhudia mwenyewe, ushuhuda wangu
ni kweli kwa sababu najua nilikotoka
na ninakokwenda. Lakini ninyi hamjui
nilikotoka wala ninakokwenda. 15 [o]Ninyi
mnahukumu kwa kufuata vipimo vya
kibinadamu, mimi simhukumu mtu yeyote.
16 [p]Lakini hata kama nikihukumu, uamuzi
wangu ni sahihi kwa sababu sitoi hukumu
yangu peke yangu, bali niko pamoja na
Baba, aliyenituma. 17 Imeandikwa katika
Sheria yenu kwamba, ushahidi wa watu
wawili ni thabiti. 18 [q]Mimi najishuhudia
mwenyewe, naye Baba aliyenituma
hunishuhudia."
19 [r]Ndipo wakamuuliza, "Huyo Baba yako
yuko wapi?"
Yesu akawajibu, "Ninyi hamnifahamu
mimi ni nani, wala hammfahamu Baba
yangu. Kama mngenifahamu mimi,
mngemfahamu na Baba yangu." 20 [s]Yesu
alisema maneno haya alipokuwa akifundisha
katika chumba cha hazina Hekaluni. Lakini

[a]**7:48** Yn 12:42
[b]**7:50** Yn 3:1
[c]**7:51** Kum 1:16, 17; 19:15
[d]**7:52** Yn 1:46; 7:41
[e]**8:1** Mt 21:1
[f]**8:2** Mt 26:55
[g]**8:5** Kum 22:22; Ay 31:11
[h]**8:6** Mt 22:15-18; 12:10
[i]**8:7** Kum 17:7; Eze 16:40; Rum 2:1, 22
[j]**8:9** Rum 2:22
[k]**8:11** Yn 3:17; 5:14
[l]**8:12** Yn 6:35; 12:35; Mit 4:18; Mt 5:14
[m]**8:13** Yn 5:31
[n]**8:14** Yn 13:3; 16:28; 7:28; 9:29
[o]**8:15** Yn 7:24; 3:17
[p]**8:16** Yn 5:30
[q]**8:18** Yn 5:37
[r]**8:19** Yn 16:3; 14:7; 1Yn 2:23
[s]**8:20** Mt 26:18, 55; Mk 12:41; Yn 7:30

hakuna mtu aliyemkamata kwa kuwa saa
yake ilikuwa haijawadia.

*Yesu Atabiri Kifo Chake Mwenyewe*

21 [a]Yesu akawaambia tena, “Ninaenda
zangu, nanyi mtanitafuta, lakini mtakufa
katika dhambi zenu. Niendako mimi ninyi
hamwezi kuja.”
22 [b]Ndipo wale Wayahudi wakasema, “Je,
atajiua? Je, hii ndiyo sababu amesema,
‘Niendako mimi ninyi hamwezi kuja’?”
23 [c]Akawaambia, “Ninyi mmetoka
chini, mimi nimetoka juu. Ninyi ni wa
ulimwengu huu, mimi si wa ulimwengu
huu. 24 [d]Niliwaambia kuwa mtakufa katika
dhambi zenu, kwa maana msipoamini ya
kwamba ‘Mimi Ndiye,’ mtakufa katika
dhambi zenu.”
25 [e]Wakamuuliza, “Wewe ni nani?”
Naye Yesu akawajibu, “Mimi ndiye yule
ambaye nimekuwa nikiwaambia tangu
mwanzo. 26 [f]Nina mambo mengi ya kusema
juu yenu na mengi ya kuwahukumu. Lakini
yeye aliyenituma ni wa kweli, nami nanena
na ulimwengu niliyoyasikia kutoka kwake.”
27 Hawakuelewa kuwa alikuwa
akiwaambia juu ya Baba yake wa
Mbinguni. 28 [g]Kisha Yesu akawaambia,
“Mtakapokwisha kumwinua juu Mwana
wa Adamu, ndipo mtakapojua kuwa,
‘Mimi ndiye yule niliyesema na kwamba
mimi sitendi jambo lolote peke yangu
bali ninasema yale tu ambayo Baba yangu
amenifundisha. 29 [h]Yeye aliyenituma yu
pamoja nami, hajaniacha, kwa kuwa siku
zote nafanya mapenzi yake.’ ” 30 [i]Wengi
waliomsikia Yesu akisema maneno haya
wakamwamini.

*Wanafunzi Wa Kweli*

31 [j]Kisha Yesu akawaambia wale
Wayahudi waliomwamini, “Kama mkidumu
katika maneno yangu, mtakuwa wanafunzi
wangu kweli kweli. 32 [k]Ndipo mtaijua kweli
nayo kweli itawaweka huru.”
33 [l]Wao wakamjibu, “Sisi tu wazao wa
Abrahamu, nasi hatujawa watumwa wa
mtu yeyote. Wawezaje kusema kwamba
tutawekwa huru?”
34 [m]Yesu akajibu, “Amin, amin nawaambia,
kila atendaye dhambi ni mtumwa wa
dhambi. 35 [n]Mtumwa hakai nyumbani
anakotumika siku zote, lakini mwana
hukaa nyumbani daima. 36 [o]Hivyo Mwana
akiwaweka huru mtakuwa huru kweli
kweli. 37 [p]Ninajua ya kuwa ninyi ni wazao
wa Abrahamu, lakini mnatafuta wasaa wa
kuniua kwa sababu ndani yenu hamna
nafasi ya neno langu. 38 [q]Ninasema yale
niliyoyaona mbele za Baba yangu, nanyi
inawapa kufanya yale mliyosikia kutoka
kwa baba yenu.”

*Yesu Na Abrahamu*

39 [r]Wakajibu, “Baba yetu ni Abrahamu.”
Yesu akawaambia, “Kama mngekuwa
wazao wa Abrahamu mngefanya mambo
yale aliyofanya Abrahamu. 40 [s]Lakini sasa
ninyi mnatafuta kuniua, mtu ambaye
nimewaambia kweli ile niliyosikia kutoka
kwa Mungu, Abrahamu hakufanya jambo
la namna hii. 41 [t]Ninyi mnafanya mambo
afanyayo baba yenu.”
Wakamjibu, “Sisi hatukuzaliwa kwa
uzinzi. Tunaye Baba mmoja, Mungu pekee.”
42 [u]Yesu akawaambia, “Kama Mungu
angekuwa Baba yenu, mngenipenda, kwa
maana nilitoka kwa Mungu na sasa niko

[a]**8:21** Eze 3:18; Yn 7:34; 13:33
[b]**8:22** Yn 7:35
[c]**8:23** Yn 3:31; 17:14
[d]**8:24** Yn 4:26; 13:19
[e]**8:25** Yn 8:14
[f]**8:26** Yn 7:28; 3:32; 15:15
[g]**8:28** Yn 3:14; 5:19
[h]**8:29** Yn 16:32; Isa 50:5; Yn 4:34
[i]**8:30** Yn 7:31
[j]**8:31** Yn 15:7; 2Yn 9
[k]**8:32** Gal 5:1, 13; Yak 2:12
[l]**8:33** Mk 3:9; Lk 3:8
[m]**8:34** Rum 6:16; 2Pet 2:19
[n]**8:35** Gal 4:30
[o]**8:36** Rum 8:2; Gal 5:1
[p]**8:37** Yn 7:19; 8:40
[q]**8:38** Yn 5:19, 30; 14:10, 24
[r]**8:39** Lk 3:8; Gal 3:7
[s]**8:40** Yn 8:37; 8:26
[t]**8:41** Isa 63:16; 64:8; Mal 1:6
[u]**8:42** 1Yn 5:1; Yn 16:27; 7:28; 3:17

hapa. Sikuja kwa ajili yangu mwenyewe,
ila yeye alinituma. 43 [a]Kwa nini hamwelewi
ninayowaambia? Ni kwa sababu hamwezi
kusikia nisemacho. 44 [b]Ninyi ni watoto wa
baba yenu ibilisi, nanyi mnataka kutimiza
matakwa ya baba yenu. Yeye alikuwa muuaji
tangu mwanzo, wala hakushikana na kweli
maana hamna kweli ndani yake. Asemapo
uongo husema yaliyo yake mwenyewe kwa
maana yeye ni mwongo na baba wa huo
uongo. 45 [c]Lakini kwa sababu nimewaambia
kweli hamkuniamini! 46 [d]Je, kuna yeyote
miongoni mwenu awezaye kunithibitisha
kuwa mwenye dhambi? Kama nawaambia
yaliyo kweli, mbona hamniamini? 47 [e]Yeye
atokaye kwa Mungu husikia kile Mungu
asemacho. Sababu ya ninyi kutosikia ni kwa
kuwa hamtokani na Mungu."

*Maelezo Ya Yesu Kuhusu Yeye Mwenyewe*

48 [f]Wayahudi wakamjibu Yesu, "Je,
hatuko sahihi tunaposema ya kwamba
wewe ni Msamaria na ya kwamba una pepo
mchafu?"

49 Yesu akawajibu, "Mimi sina pepo
mchafu, bali ninamheshimu Baba yangu,
nanyi mnanidharau. 50 [g]Lakini mimi
sitafuti utukufu wangu mwenyewe, bali
yuko anayetaka kunitukuza, naye ndiye
mwamuzi. 51 [h]Amin, amin nawaambia, mtu
yeyote akilitii neno langu hataona mauti
milele."

52 [i]Ndipo Wayahudi wakamwambia,
"Sasa tumejua kwamba una pepo mchafu.
Ikiwa Abrahamu alikufa na vivyo hivyo
manabii, nawe unasema 'Mtu akitii neno
langu hatakufa milele.' 53 [j]Je, wewe ni mkuu
kuliko baba yetu Abrahamu ambaye alikufa
na manabii ambao nao pia walikufa? Hivi
wewe unajifanya kuwa nani?"

54 [k]Yesu akawajibu, "Kama nikijitukuza
utukufu wangu hauna maana. Baba yangu,
huyo ambaye ninyi mnadai kuwa ni Mungu
wenu, ndiye anitukuzaye mimi. 55 [l]Ingawa
hamkumjua, mimi ninamjua. Kama
ningesema simjui, ningekuwa mwongo
kama ninyi, lakini mimi ninamjua na
ninalitii neno lake. 56 [m]Baba yenu Abrahamu
alishangilia kwamba angaliiona siku yangu,
naye akaiona na akafurahi."

57 Wayahudi wakamwambia, "Wewe
hujatimiza hata miaka hamsini, wewe
wasema umemwona Abrahamu?"

58 [n]Yesu akawaambia, "Amin, amin
nawaambia, kabla Abrahamu hajakuwako,
'Mimi niko.' " 59 [o]Ndipo wakaokota mawe
ili kumpiga, lakini Yesu akajificha, naye
akatoka Hekaluni.

*Yesu Amponya Mtu Aliyezaliwa Kipofu*

9 [p]Yesu alipokuwa akipita, akamwona
mtu aliyekuwa kipofu tangu kuzaliwa.
2 [q]Wanafunzi wake wakamuuliza, "Rabi, ni
nani aliyetenda dhambi, ni huyu mtu au
wazazi wake hata azaliwe kipofu?"

3 [r]Yesu akawajibu, "Huyu mtu wala wazazi
wake hawakutenda dhambi. Alizaliwa
kipofu ili kazi za Mungu zidhihirishwe
katika maisha yake. 4 [s]Yanipasa kuzifanya
kazi zake yeye aliyenituma wakati bado
ni mchana, kwa kuwa usiku waja ambapo
hakuna mtu awezaye kufanya kazi.
5 [t]Wakati niko ulimwenguni, mimi ni nuru
ya ulimwengu."

6 [u]Baada ya kusema haya, akatema mate
ardhini, akatengeneza tope kwa mate na
kumpaka yule mtu kipofu machoni. 7 [v]Kisha
akamwambia, "Nenda ukanawe katika

[a]**8:43** Yn 7:17
[b]**8:44** 1Yn 3:8; 2Nya 18:21; Za 12:2
[c]**8:45** Yn 18:37
[d]**8:46** 2Kor 5:21; 1Pet 2:22
[e]**8:47** Yn 18:37; 1Yn 4:6
[f]**8:48** Mt 10:5; Mk 3:22; Yn 7:20
[g]**8:50** Yn 7:20; 8:54; 10:20
[h]**8:51** Yn 11:26
[i]**8:52** Zek 1:5; Ebr 11:13
[j]**8:53** Yn 4:12
[k]**8:54** Yn 16:14; 17:1-5
[l]**8:55** Yn 7:28-29; 15:10
[m]**8:56** Mwa 18:18; Mt 13:17; Ebr 11:13
[n]**8:58** Yn 1:2; 17:5, 24; Kut 3:14; 6:3
[o]**8:59** 1Sam 30:6; Yn 11:8; 12:36
[p]**9:1** Mdo 3:2; 14:8
[q]**9:2** Lk 13:2; Mdo 28:4; Eze 18:20; Kut 20:5; Ay 21:19
[r]**9:3** Yn 11:14
[s]**9:4** Yn 1:9; 12:35
[t]**9:5** Yn 8:12
[u]**9:6** Mk 7:33; 8:23
[v]**9:7** 2Fal 5:10; Lk 13:4; Isa 35:5; Yn 11:37

bwawa la Siloamu." (Siloamu maana yake
ni aliyetumwa.) Ndipo yule kipofu akaenda,
akanawa, naye akarudi akiwa anaona.
8 [a]Majirani zake na wale wote waliokuwa
wamemwona hapo awali akiombaomba
wakaanza kuuliza, "Je, huyu si yule
aliyekuwa akiketi akiombaomba?"
9 Wengine wakasema, "Ndiye."

Wengine wakasema, "Siye, bali
wamefanana."

Lakini yeye akawaambia, "Mimi ndiye."
10 Wakamuuliza, "Basi macho yako
yalifumbuliwaje?"
11 [b]Yeye akawajibu, "Yule mtu aitwaye
Yesu alitengeneza tope, akanipaka machoni
mwangu, naye akaniambia nenda ukanawe
katika Bwawa la Siloamu, ndipo nikanawa
nami nikapata kuona!"
12 Wale wakamuuliza, "Yeye huyo mtu
yuko wapi?"

Akawajibu, "Sijui."

*Mafarisayo Wachunguza Kuponywa Kwa Kipofu*

13 Wakamleta kwa Mafarisayo yule
mtu aliyekuwa kipofu hapo awali. 14 [c]Basi
siku hiyo Yesu alipotengeneza tope na
kuyafungua macho ya huyo mtu ilikuwa
Sabato. 15 Mafarisayo nao wakaanza
kumuuliza alivyopata kuponywa. Naye
akawaambia, "Alinipaka tope kwenye
macho yangu, nikanawa na sasa ninaona."
16 [d]Baadhi ya Mafarisayo wakasema,
"Huyu mtu hatoki kwa Mungu, kwa sababu
hashiki Sabato."

Lakini wengine wakasema, "Awezaje mtu
mwenye dhambi kufanya miujiza kama
hii?" Wakagawanyika.
17 [e]Hivyo wakamwambia tena yule
mtu aliyekuwa kipofu, "Wewe ndiwe
uliyefumbuliwa macho, wasemaje kuhusu
mtu huyo?" Maana macho yako ndiyo
yaliyofumbuliwa.

Yeye akawajibu, "Yeye ni nabii."

18 [f]Wale Wayahudi hawakuamini ya
kuwa mtu huyo alikuwa kipofu, akapata
kuona, mpaka walipowaita wazazi wake.
19 Wakawauliza, "Je, huyu ni mtoto wenu,
ambaye mnasema alizaliwa kipofu?
Imekuwaje basi sasa anaona?"
20 Wazazi wake wakajibu, "Tunajua ya
kuwa huyu ni mtoto wetu na ya kuwa
alizaliwa kipofu. 21 Lakini sisi hatujui ni
kwa jinsi gani kwamba sasa anaona, wala
hatujui ni nani aliyemfungua macho yake.
Muulizeni, yeye ni mtu mzima na anaweza
kujieleza mwenyewe." 22 [g]Wazazi wake
walisema hivi kwa sababu waliwaogopa
Wayahudi kwani walikuwa wamekubaliana
kuwa mtu yeyote atakayemkiri Yesu kuwa
ndiye Kristo[h] atafukuzwa kutoka sinagogi.
23 [i]Kwa hiyo wazazi wake wakasema, "Yeye
ni mtu mzima. Muulizeni."
24 [j]Hivyo kwa mara ya pili wakamwita
yule aliyekuwa kipofu, nao wakamwambia,
"Mpe Mungu utukufu! Sisi tunafahamu
kuwa mtu huyu aliyekuponya ni mwenye
dhambi."
25 Akawajibu, "Mimi sijui kama yeye
ni mwenye dhambi. Lakini jambo moja
ninalojua, nilikuwa kipofu na sasa ninaona."
26 Wakamuuliza, "Alikufanyia nini?
Aliyafumbuaje macho yako?"
27 [k]Akawajibu, "Tayari nimekwisha
kuwaambia, nanyi hamtaki kunisikiliza.
Mbona mnataka kusikia tena? Je, ninyi
nanyi mnataka kuwa wanafunzi wake?"
28 [l]Ndipo wakamtukana na kusema,
"Wewe ndiwe mwanafunzi wake, Sisi ni
wanafunzi wa Mose. 29 [m]Tunajua kwamba
Mungu alisema na Mose, lakini kwa habari
ya mtu huyu hatujui atokako."
30 [n]Yule mtu akawajibu, "Hili ni jambo
la ajabu! Hamjui anakotoka, naye

[a]**9:8** Mdo 3:2-10
[b]**9:11** Yn 9:6, 7
[c]**9:14** Mt 12:1-14; Yn 5:9
[d]**9:16** Mt 12:2; Yn 7:43; 10:19
[e]**9:17** Mt 21:11; Yn 4:19
[f]**9:18** Yn 1:19
[g]**9:22** Yn 7:13; Lk 6:22; Yn 16:2; 12:42
[h]22 *Kristo* maana yake ni *Masiya*, yaani *Aliyetiwa mafuta.*
[i]**9:23** Yn 9:21
[j]**9:24** Yos 7:19
[k]**9:27** Yn 9:15
[l]**9:28** Yn 5:45
[m]**9:29** Yn 8:14
[n]**9:30** Yn 3:10

amenifungua macho yangu! 31 [a]Tunajua ya
kuwa Mungu hawasikilizi wenye dhambi,
lakini huwasikiliza wote wanaomcha na
kumtii. 32 Tangu zamani hatujasikia kwamba
mtu amemponya yeyote aliyezaliwa kipofu.
33 [b]Kama huyu mtu hakutoka kwa Mungu,
asingeweza kufanya lolote."
34 [c]Wao wakamjibu, "Wewe ulizaliwa
katika dhambi kabisa, nawe unajaribu
kutufundisha?" Wakamfukuza atoke nje.

*Upofu Wa Kiroho*

35 [d]Yesu aliposikia kuwa wamemfukuzia
nje yule mtu aliyemfumbua macho,
alimkuta akamuuliza, "Je, unamwamini
Mwana wa Adamu?"
36 [e]Yule mtu akamjibu, "Yeye ni nani,
Bwana? Niambie ili nipate kumwamini."
37 [f]Yesu akamjibu, "Umekwisha kumwona,
naye anayezungumza nawe, ndiye."
38 [g]Yule mtu akasema, "Bwana, naamini."
Naye akamwabudu.
39 [h]Yesu akasema, "Nimekuja ulimwenguni
humu kwa ajili ya kuhukumu, ili wale walio
vipofu wapate kuona, nao wale wanaoona,
wawe vipofu."
40 [i]Baadhi ya Mafarisayo waliokuwa
karibu naye wakamsikia na kumwambia,
"Je, kweli sisi ni vipofu?"
41 [j]Yesu akawajibu, "Kama mngekuwa
vipofu kweli, msingekuwa na hatia ya
dhambi, lakini kwa kuwa mnasema,
'Tunaona,' basi mna hatia.

*Mchungaji Mwema*

10 [k]"Amin, amin nawaambia, yeye
asiyeingia katika zizi la kondoo
kwa kupitia kwenye lango, lakini akwea
kuingia ndani kwa njia nyingine, ni mwizi
na mnyang'anyi. 2 [l]Yeye anayeingia kwa
kupitia kwenye lango ndiye mchungaji
wa kondoo. 3 [m]Mlinzi humfungulia lango
na kondoo huisikia sauti yake. Huwaita
kondoo wake kwa majina yao na kuwatoa
nje ya zizi. 4 [n]Akiisha kuwatoa wote
nje, hutangulia mbele yao na kondoo
humfuata kwa kuwa wanaijua sauti yake.
5 [o]Lakini kondoo hawatamfuata mgeni bali
watamkimbia, kwa sababu hawaijui sauti
ya mgeni." 6 [p]Yesu alitumia mfano huu,
lakini wao hawakuelewa hayo aliyokuwa
akiwaambia.
7 [q]Kwa hiyo Yesu akasema nao tena
akawaambia, "Amin, amin nawaambia,
mimi ndimi lango la kondoo. 8 [r]Wote
walionitangulia ni wevi na wanyang'anyi,
lakini kondoo hawakuwasikia. 9 [s]Mimi
ndimi lango, yeyote anayeingia zizini kwa
kupitia kwangu ataokoka, ataingia na
kutoka, naye atapata malisho. 10 [t]Mwizi
huja ili aibe, kuua na kuangamiza. Mimi
nimekuja ili wapate uzima kisha wawe nao
tele.
11 [u]"Mimi ndimi mchungaji mwema.
Mchungaji mwema huutoa uhai wake kwa
ajili ya kondoo. 12 [v]Mtu wa kuajiriwa sio
mchungaji mwenye kondoo. Amwonapo
mbwa mwitu akija, yeye hukimbia na
kuwaacha kondoo. Naye mbwa mwitu
hulishambulia kundi na kulitawanya.
13 Yeye hukimbia kwa sababu ameajiriwa
wala hawajali kondoo.
14 [w]"Mimi ndimi mchungaji mwema.
Ninawajua kondoo wangu nao kondoo
wangu wananijua. 15 [x]Kama vile Baba
anavyonijua mimi, nami ninavyomjua

---

[a]**9:31** Za 66:18; Yak 5:16-18
[b]**9:33** Yn 3:2
[c]**9:34** Isa 66:5
[d]**9:35** Mt 14:33; 16:16; Mk 1:1; 1Yn 5:13
[e]**9:36** Rum 10:14
[f]**9:37** Yn 4:26
[g]**9:38** Mt 28:9
[h]**9:39** Yn 5:22; 3:19; 12:47; Lk 4:18; Mt 13:13
[i]**9:40** Rum 2:19
[j]**9:41** Yn 15:22-24
[k]**10:1** Yn 10:8, 10
[l]**10:2** Mk 6:34; Yn 10:11, 14
[m]**10:3** Yn 10:4, 5, 14
[n]**10:4** Yn 10:3
[o]**10:5** Yn 10:27
[p]**10:6** Yn 16:25; 16:25
[q]**10:7** Za 118:20; Yn 14:6; Mt 7:13; 14
[r]**10:8** Yer 23:1-2; Eze 34:2
[s]**10:9** Za 118:20; Yn 14:6; 1Kor 3:15
[t]**10:10** Yn 1:4; 3:15, 16; 5:40; 20:31; Za 65:11; Rum 5:17
[u]**10:11** Za 23:1; Mt 2:6; Yn 15:13; 1Yn 3:16
[v]**10:12** Zek 11:16-17
[w]**10:14** Kut 33:12; 2Tim 2:19
[x]**10:15** Mt 11:27; Yn 15:16

Baba, nami nautoa uhai wangu kwa ajili ya
kondoo. 16 [a]Ninao kondoo wengine ambao
si wa zizi hili, inanipasa kuwaleta, nao
wataisikia sauti yangu, hivyo patakuwa na
kundi moja na mchungaji mmoja. 17 [b]Baba
yangu ananipenda kwa kuwa ninautoa uhai
wangu ili niupate tena. 18 [c]Hakuna mtu
aniondoleaye uhai wangu, bali ninautoa
kwa hiari yangu mwenyewe. Ninao uwezo
wa kuutoa uhai wangu na pia ninao uwezo
wa kuutwaa tena. Amri hii nimepewa na
Baba yangu."

19 [d]Kwa maneno haya Wayahudi
waligawanyika. 20 [e]Wengi wao wakasema,
"Huyu amepagawa na pepo mchafu, naye
amechanganyikiwa."

21 [f]Wengine wakasema, "Haya si maneno
ya mtu aliyepagawa na pepo mchafu. Je,
pepo mchafu aweza kufungua macho ya
kipofu?"

*Yesu Akataliwa Na Wayahudi*

22 Wakati huo ilikuwa Sikukuu ya
Kuwekwa wakfu kwa Hekalu[g] huko
Yerusalemu, nao ulikuwa wakati wa majira
ya baridi. 23 [h]Naye Yesu alikuwa akitembea
ndani ya Hekalu katika ukumbi wa
Solomoni. 24 [i]Wayahudi wakamkusanyikia
wakamuuliza, "Utatuweka katika hali ya
mashaka mpaka lini? Kama wewe ndiye
Kristo[j] tuambie waziwazi."

25 [k]Yesu akawajibu, "Nimewaambia,
lakini hamwamini. Mambo ninayoyatenda
kwa jina la Baba yangu yananishuhudia.
26 [l]Lakini hamwamini, kwa sababu ninyi
si wa kundi la kondoo wangu. 27 [m]Kondoo
wangu huisikia sauti yangu nami nawajua,
nao hunifuata, 28 [n]nami ninawapa uzima
wa milele, hawataangamia kamwe wala
hakuna mtu atakayewapokonya kutoka
mikono yangu. 29 [o]Baba yangu aliyenipa
hawa ni mkuu kuliko wote na hakuna
awezaye kuwapokonya kutoka mikononi
mwake. 30 [p]Mimi na Baba yangu tu umoja."

31 [q]Kwa mara nyingine Wayahudi
wakainua mawe ili wampige nayo, 32 lakini
Yesu akawaambia, "Nimewaonyesha
miujiza mingi mikubwa kutoka kwa Baba
yangu. Ni ipi katika hiyo mnataka kunipiga
mawe?"

33 [r]Wayahudi wakamjibu, "Hatukupigi
mawe kwa sababu ya mambo mema
uliyotenda, bali ni kwa kuwa umekufuru.
Wewe ingawa ni mwanadamu unajifanya
kuwa Mungu."

34 [s]Yesu akawajibu, "Je, haikuandikwa
katika Sheria ya kwamba, 'Nimesema
kuwa, ninyi ni miungu?' 35 [t]Kama aliwaita
'miungu,' wale ambao neno la Mungu
liliwafikia, nayo Maandiko hayawezi
kutanguka, 36 [u]je, mwawezaje kusema
kwamba yule ambaye Baba amemweka
wakfu na kumtuma ulimwenguni
anakufuru, kwa sababu nilisema, 'Mimi ni
Mwana wa Mungu?' 37 [v]Ikiwa sifanyi kazi
za Baba yangu, basi msiniamini, 38 [w]lakini
ikiwa nazifanya kazi za Mungu, hata kama
hamniamini mimi ziamininі hizo kazi, ili
mpate kujua na kuelewa kwamba Baba yu
ndani yangu, nami ndani yake." 39 [x]Ndipo
wakajaribu kumkamata kwa mara nyingine,
lakini akaponyoka kutoka mikononi mwao.

40 [y]Akaenda tena ng'ambo ya Mto Yordani

---

[a]**10:16** Isa 56:8; Mdo 10:34-35; Yn 17:20-21; Efe 2:11-19; Eze 34:23; 1Pet 2:25
[b]**10:17** Isa 53:7, 8, 12; Ebr 2:9
[c]**10:18** Mt 26:53; Flp 2:8; Ebr 5:8
[d]**10:19** Yn 6:52
[e]**10:20** Mk 3:22; Yn 7:20; 2Fal 9:11
[f]**10:21** Mt 4:24; Kut 4:11; Yn 9:32-33
[g]22 Sikukuu ya Kuwekwa wakfu kwa Hekalu ni Hanukkah kwa Kiebrania.
[h]**10:23** Mdo 3:11; 5:12
[i]**10:24** Yn 1:19; Lk 22:67
[j]24 *Kristo* maana yake ni *Masiya*, yaani *Aliyetiwa mafuta.*
[k]**10:25** Yn 4:26; 4:11
[l]**10:26** Yn 8:47
[m]**10:27** Yn 10:4, 14
[n]**10:28** Yn 6:39
[o]**10:29** Yn 17:2, 6, 24; 14:28
[p]**10:30** Kum 6:4; Yn 17:21-24
[q]**10:31** Yn 8:59
[r]**10:33** Law 24:16; Mt 26:63-66
[s]**10:34** Rum 3:19; 1Kor 14:21; Za 82:6
[t]**10:35** Rum 13:1; Mt 5:17, 18
[u]**10:36** Yer 1:5; Yn 6:69; 3:17
[v]**10:37** Yn 15:24
[w]**10:38** Yn 14:10-11; 20:17-21
[x]**10:39** Yn 7:30; Lk 4:30; Yn 8:59
[y]**10:40** Yn 1:28

mpaka mahali pale ambapo Yohana alikuwa
akibatiza hapo awali, naye akakaa huko.
41 [a]Watu wengi wakamjia, nao wakawa
wakisema, "Yohana hakufanya muujiza
wowote, lakini kila jambo alilosema
kumhusu huyu mtu ni kweli." 42 [b]Nao wengi
wakamwamini Yesu huko.

*Kifo Cha Lazaro*

11 [c]Basi mtu mmoja jina lake Lazaro
alikuwa mgonjwa. Yeye alikuwa
akiishi Bethania kijiji cha Maria na Martha
dada zake. 2 [d]Huyu Maria, ambaye Lazaro
kaka yake alikuwa mgonjwa, ndiye yule
ambaye alimpaka Bwana mafuta na kuifuta
miguu yake kwa nywele zake. 3 [e]Hivyo hawa
dada wawili walituma ujumbe kwa Yesu
kumwambia, "Bwana, yule umpendaye ni
mgonjwa."
4 [f]Lakini Yesu aliposikia hayo, akasema,
"Ugonjwa huu hautaleta mauti bali
umetokea ili kudhihirisha utukufu wa
Mungu, ili Mwana wa Mungu apate
kutukuzwa kutokana na ugonjwa huu."
5 Pamoja na hivyo, ingawa Yesu aliwapenda
Martha, Maria na Lazaro ndugu yao, 6 [g]baada
ya kusikia kwamba Lazaro ni mgonjwa,
aliendelea kukawia huko alikokuwa kwa
siku mbili zaidi.
7 [h]Ndipo akawaambia wanafunzi wake,
"Haya, turudi Uyahudi."
8 [i]Wanafunzi wake wakamwambia, "Rabi,
Wayahudi walikuwa wanataka kukupiga
mawe, nawe unataka kurudi huko?"
9 [j]Yesu akawajibu, "Si kuna saa kumi na
mbili za mchana katika siku moja? Wala
watembeao mchana hawawezi kujikwaa
kwa maana wanaona nuru ya ulimwengu
huu. 10 [k]Lakini wale watembeao usiku
hujikwaa kwa sababu hakuna nuru ndani
yao."
11 [l]Baada ya kusema haya, Yesu
akawaambia, "Rafiki yetu Lazaro amelala,
lakini naenda kumwamsha."
12 Wanafunzi wakamwambia, "Bwana,
kama amelala usingizi ataamka." 13 [m]Hata
hivyo, Yesu alikuwa anazungumzia kuwa
Lazaro amekufa, lakini wanafunzi wake
hawakuelewa, walidhani kwamba anasema
Lazaro amelala usingizi tu.
14 Kwa hiyo Yesu akawaambia waziwazi,
"Lazaro amekufa. 15 Hata hivyo nafurahi
kwa kuwa sikuwepo huko kabla ya Lazaro
kufa, ili mpate kuamini. Lakini sasa
twendeni kwake."
16 [n]Tomaso aliyeitwa Pacha akawaambia
wanafunzi wenzake, "Sisi nasi twendeni
tukafe pamoja naye."

*Yesu Ndiye Ufufuo Na Uzima*

17 [o]Yesu alipowasili huko alikuta Lazaro
amekuwa kaburini siku nne. 18 [p]Basi Bethania
ulikuwa karibu na Yerusalemu umbali wa
karibu maili mbili,[q] 19 [r]na Wayahudi wengi
walikuwa wamekuja kuwafariji Martha na
Maria kwa ajili ya kufiwa na ndugu yao.
20 [s]Martha aliposikia kwamba Yesu anakuja,
alitoka kwenda kumlaki, ila Maria alibaki
nyumbani.
21 [t]Martha akamwambia Yesu, "Bwana,
kama ungalikuwa hapa, ndugu yangu
hangalikufa. 22 [u]Lakini sasa ninajua kuwa
chochote utakachomwomba Mungu,
atakupa."
23 Yesu akamwambia, "Ndugu yako
atafufuka."
24 [v]Martha akamjibu, "Ninajua ya kuwa

[a]**10:41** Yn 2:1; 1:26-34
[b]**10:42** Yn 7:31
[c]**11:1** Mt 21:17; Lk 10:38
[d]**11:2** Mk 14:3; Lk 7:38
[e]**11:3** Yn 11:5, 36
[f]**11:4** Yn 11:40
[g]**11:6** Yn 10:40
[h]**11:7** Yn 10:40
[i]**11:8** Mt 23:7; Yn 8:59; 10:31
[j]**11:9** Yn 9:4; 12:35
[k]**11:10** Yn 12:35
[l]**11:11** Mt 9:24; Lk 8:52
[m]**11:13** Mt 9:24
[n]**11:16** Mt 10:3; Mdo 1:13
[o]**11:17** Yn 11:6, 39
[p]**11:18** Yn 11:1; Mt 21:17
[q]18 Maili mbili ni kama kilomita tatu.
[r]**11:19** Yn 11:31; Ay 2:11
[s]**11:20** Lk 10:38-42
[t]**11:21** Yn 11:32, 37
[u]**11:22** Yn 11:41, 42
[v]**11:24** Dan 12:2; Mdo 24:15

atafufuka wakati wa ufufuo wa wafu siku
ya mwisho."
25 [a]Yesu akamwambia, "Mimi ndiye huo
ufufuo na uzima. Yeye aniaminiye mimi,
hata akifa atakuwa anaishi 26 [b]na yeyote
aishiye na kuniamini hatakufa kabisa hata
milele. Je, unasadiki haya?"
27 [c]Martha akamwambia, "Ndiyo
Bwana, ninaamini ya kuwa wewe ndiwe
Kristo,[d] Mwana wa Mungu, yeye ajaye
ulimwenguni."

*Yesu Alia*

28 [e]Baada ya kusema haya Martha
alikwenda, akamwita Maria dada yake
faraghani na kumwambia, "Mwalimu
yuko hapa anakuita." 29 Maria aliposikia
hivyo, akaondoka upesi akaenda mpaka
alipokuwa Yesu. 30 [f]Yesu alikuwa hajaingia
kijijini, bali alikuwa bado yuko mahali pale
alipokutana na Martha. 31 [g]Wale Wayahudi
waliokuwa pamoja na Maria nyumbani
wakimfariji walipoona ameondoka haraka
na kutoka nje, walimfuata wakidhani ya
kwamba alikuwa anakwenda kule kaburini
kulilia huko.
32 [h]Maria alipofika mahali pale Yesu
alipokuwa, alipiga magoti miguuni Pake na
kusema, "Bwana, kama ungalikuwa hapa,
ndugu yangu hangalikufa."
33 [i]Yesu alipomwona Maria akilia na
wale Wayahudi waliokuja pamoja naye
pia wakilia, Yesu alisikia uchungu moyoni,
akafadhaika sana. 34 Akauliza, "Mmemweka
wapi?"
Wakamwambia, "Bwana, njoo upaone."
35 [j]Yesu akalia machozi.
36 [k]Ndipo Wayahudi wakasema, "Tazama
jinsi alivyompenda Lazaro!"
37 [l]Lakini wengine wakasema, "Je, yule
aliyefungua macho ya kipofu, hakuweza
kumfanya na huyu asife?"

*Yesu Amfufua Lazaro*

38 [m]Yesu kwa mara nyingine akiwa
amefadhaika sana, akafika penye kaburi.
Hilo kaburi lilikuwa pango ambalo jiwe
lilikuwa limewekwa kwenye ingilio lake.
39 [n]Yesu akasema, "Liondoeni hilo jiwe."
Martha ndugu yake yule aliyekuwa
amekufa akasema, "Lakini Bwana, wakati
huu atakuwa ananuka kwani amekwisha
kuwa kaburini siku nne."
40 [o]Yesu akamwambia, "Sikukuambia
kwamba kama ukiamini utauona utukufu
wa Mungu?"
41 [p]Kwa hiyo wakaliondoa lile jiwe
kutoka kaburini. Yesu akainua macho
yake juu akasema, "Baba, ninakushukuru
kwa kuwa wanisikia. 42 [q]Ninajua ya kuwa
wewe hunisikia siku zote, lakini nimesema
haya kwa ajili ya umati huu uliosimama
hapa, ili wapate kuamini ya kuwa wewe
umenituma."
43 [r]Baada ya kusema haya, Yesu akapaza
sauti yake akaita, "Lazaro, njoo huku!"
44 [s]Yule aliyekuwa amekufa akatoka
nje, mikono yake na miguu yake ikiwa
imeviringishiwa vitambaa vya kitani na
leso usoni pake.
Yesu akawaambia, "Mfungueni,
mwacheni aende zake."

*Shauri La Kumuua Yesu*

**(Mathayo 26:1-5; Marko 14:1-2; Luka 22:1-2)**

45 [t]Hivyo Wayahudi wengi waliokuwa

[a]**11:25** Yn 1:4
[b]**11:26** Yn 3:15; Mt 25:46
[c]**11:27** Lk 2:11; Mt 4:3; 16:16; Yn 6:14
[d]27 *Kristo* maana yake ni *Masiya*, yaani *Aliyetiwa mafuta.*
[e]**11:28** Mt 26:18; Yn 13:13
[f]**11:30** Yn 11:20; 13:13
[g]**11:31** Yn 11:19; 8:59
[h]**11:32** Yn 11:21; 5:18
[i]**11:33** Yn 11:38; 12:27; 13:21
[j]**11:35** Lk 19:41
[k]**11:36** Yn 11:3
[l]**11:37** Yn 9:6, 7; 11:21, 32
[m]**11:38** Yn 11:33; Mt 27:60; Lk 24:2; Yn 20:1
[n]**11:39** Yn 11:17
[o]**11:40** Yn 11:23-25
[p]**11:41** Yn 17:1; Mt 11:25
[q]**11:42** Yn 12:30; 3:17
[r]**11:43** Lk 7:14
[s]**11:44** Yn 19:40; 20:7
[t]**11:45** Yn 11:19; 2:23; 14

wamekuja kumfariji Maria, walipoona yale Yesu aliyoyatenda wakamwamini. 46 Lakini baadhi yao wakaenda kwa Mafarisayo na kuwaambia mambo Yesu aliyoyafanya. 47 [a]Kwa hiyo viongozi wa makuhani na Mafarisayo wakaita mkutano wa baraza.

Wakaulizana, “Tufanyeje? Huyu mtu anafanya ishara nyingi. 48 Kama tukimwacha aendelee hivi, kila mtu atamwamini, nao Warumi watakuja na kupaharibu mahali petu patakatifu na taifa letu.”

49 [b]Mmoja wao aliyeitwa Kayafa, ambaye alikuwa kuhani mkuu mwaka huo, akasema, “Ninyi hamjui kitu chochote! 50 [c]Hamjui kwamba ni afadhali mtu mmoja afe kwa ajili ya watu, kuliko taifa lote liangamie?”

51 [d]Hakusema haya kutokana na mawazo yake mwenyewe bali kama kuhani mkuu mwaka huo, alitabiri kuwa Yesu angelikufa kwa ajili ya taifa la Wayahudi, 52 [e]wala si kwa ajili ya taifa hilo pekee, bali pia kwa ajili ya watoto wa Mungu waliotawanyika, ili kuwaleta pamoja na kuwafanya wawe wamoja. 53 [f]Hivyo tangu siku hiyo wakawa wanafanya mipango ili wamuue Yesu.

54 [g]Kwa hiyo Yesu akawa hatembei hadharani miongoni mwa Wayahudi, bali alijitenga akaenda sehemu iliyo karibu na jangwa kwenye kijiji kiitwacho Efraimu. Akakaa huko na wanafunzi wake.

55 [h]Basi Pasaka ya Wayahudi ilipokuwa imekaribia, watu wengi walitoka vijijini wakaenda Yerusalemu kabla ya Pasaka ili wakajitakase. 56 [i]Watu wakawa wanamtafuta Yesu, nao walipositimama kwenye eneo la Hekalu waliulizana, Je, mtu huyu hatakuja kamwe kwenye Sikukuu? 57 Viongozi wa makuhani na Mafarisayo walikuwa wametoa amri kuwa yeyote atakayejua mahali Yesu aliko, lazima atoe taarifa ili wapate kumkamata.

### *Maria Ampaka Yesu Mafuta Huko Bethania*

**(Mathayo 26:6-13; Marko 14:3-9)**

12 [j]Siku sita kabla ya Pasaka, Yesu alikwenda Bethania mahali ambako Lazaro aliyekuwa amefufuliwa na Yesu alikuwa anaishi. 2 [k]Wakaandaa karamu kwa heshima ya Yesu. Martha akawahudumia wakati Lazaro alikuwa miongoni mwa waliokaa mezani pamoja na Yesu. 3 [l]Kisha Maria akachukua chupa ya painti moja[m] yenye manukato ya nardo[n] safi ya thamani kubwa, akayamimina miguuni mwa Yesu na kuifuta kwa nywele zake. Nyumba nzima ikajaa harufu nzuri ya manukato.

4 [o]Ndipo Yuda Iskariote mwana wa Simoni, mmoja wa wale wanafunzi ambaye ndiye angemsaliti Yesu, akasema, 5 “Kwa nini manukato haya hayakuuzwa kwa dinari 300[p] na fedha hizo wakapewa maskini?” 6 [q]Yuda alisema hivi si kwa kuwa aliwajali maskini, bali kwa kuwa alikuwa mwizi, kwani ndiye alikuwa akitunza mfuko wa fedha akawa anaiba kile kilichowekwa humo.

7 [r]Yesu akasema, “Mwacheni. Aliyanunua manukato hayo ili ayaweke kwa ajili ya siku ya maziko yangu. 8 [s]Maskini mtakuwa nao siku zote, lakini mimi hamtakuwa nami siku zote.”

### *Shauri La Kumuua Lazaro*

9 [t]Umati mkubwa wa Wayahudi walipojua kwamba Yesu alikuwa huko

[a]**11:47** Yn 2:11
[b]**11:49** Lk 3:2; Yn 18:14; Mdo 4:6
[c]**11:50** Yn 18:14
[d]**11:51** Mwa 50:20; Kut 28:30; Hes 27:21
[e]**11:52** Isa 49:6; Yn 10:16
[f]**11:53** Mt 12:14
[g]**11:54** Yn 7:1
[h]**11:55** Kut 12:13, 23, 27; Mk 14:1; 2Nya 30:17-18
[i]**11:56** Yn 7:11; 17:7
[j]**12:1** Yn 11:55; Mt 21:17
[k]**12:2** Lk 10:38-42
[l]**12:3** Yn 11:12
[m]3 Painti moja ni kama nusu lita.
[n]3 Nardo ni aina ya mafuta yaliyokuwa yanatengenezwa kutokana na mimea yenye mizizi inayotoa harufu nzuri.
[o]**12:4** Mt 10:4
[p]5 Dinari 300 ni sawa na mshahara wa kibarua wa siku 300.
[q]**12:6** Yn 13:29
[r]**12:7** Yn 19:40
[s]**12:8** Kum 15:11
[t]**12:9** Yn 11:43, 44

Bethania, walikuja si tu kwa ajili ya Yesu,
lakini pia kumwona Lazaro ambaye Yesu
alikuwa amemfufua. 10 [a]Kwa hiyo viongozi
wa makuhani wakafanya mpango wa
kumuua Lazaro pia, 11 [b]kwa kuwa kutokana
na habari za kufufuliwa kwake Wayahudi
wengi walikuwa wanamwendea Yesu na
kumwamini.

*Kuingia Kwa Yesu Yerusalemu Kwa Ushindi*

**(Mathayo 21:1-11; Marko 1:1-11; Luka 19:28-40)**

12 [c]Siku iliyofuata umati mkubwa
uliokuwa umekuja kwenye Sikukuu
walisikia kwamba Yesu angekuja
Yerusalemu. 13 [d]Basi wakachukua matawi
ya mitende, wakatoka kwenda kumlaki,
huku wakipaza sauti wakisema,

"Hosana!"[e]

"Amebarikiwa yeye ajaye kwa Jina
la Bwana!"

"Amebarikiwa Mfalme wa Israeli!"

14 [f]Yesu akamkuta mwana-punda
akampanda, kama ilivyoandikwa,

15 [g]"Usiogope, Ewe binti Sayuni;
tazama, Mfalme wako anakuja,
amepanda mwana-punda!"

16 [h]Wanafunzi wake Yesu mwanzoni
hawakuelewa mambo haya, lakini Yesu
alipotukuzwa, ndipo walipokumbuka kuwa
mambo haya yalikuwa yameandikwa kwa
ajili yake na alitendewa yeye.
17 [i]Wale waliokuwepo wakati Yesu
alipomwita Lazaro kutoka kaburini na
kumfufua kutoka kwa wafu, waliendelea
kushuhudia. 18 [j]Ni kwa sababu pia walikuwa
wamesikia kwamba alikuwa ametenda
muujiza huu ndiyo maana umati wa watu
ukaenda kumlaki. 19 [k]Hivyo Mafarisayo
walipoona hayo wakaambiana, "Mnaona,
hamwezi kufanya lolote. Angalieni,
ulimwengu wote unamfuata yeye!"

*Yesu Anatabiri Kifo Chake*

20 [l]Basi palikuwa Wayunani fulani
miongoni mwa wale waliokuwa
wamekwenda kuabudu wakati wa Sikukuu.
21 [m]Hawa wakamjia Filipo, ambaye alikuwa
mwenyeji wa Bethsaida huko Galilaya,
wakiwa na ombi. Wakamwambia,
"Tungependa kumwona Yesu." 22 Filipo
akaenda akamweleza Andrea, nao wote
wawili wakamwambia Yesu.
23 [n]Yesu akawajibu, "Saa imewadia ya
Mwana wa Adamu kutukuzwa. 24 [o]Amin,
amin nawaambia, mbegu ya ngano
isipoanguka ardhini na kufa, hubakia kama
mbegu peke yake. Lakini ikifa huzaa mbegu
nyingi. 25 [p]Mtu yeyote anayependa maisha
yake atayapoteza, naye ayachukiaye maisha
yake katika ulimwengu huu atayaokoa
hata kwa uzima wa milele. 26 [q]Mtu yeyote
akinitumikia lazima anifuate, nami
mahali nilipo ndipo mtumishi wangu
atakapokuwa. Mtu akinitumikia, Baba
yangu atamheshimu.
27 [r]"Sasa roho yangu imefadhaika sana.
Niseme nini? 'Baba, niokoe katika saa hii.'
Lakini ni kwa kusudi hili nimeufikia wakati
huu. 28 [s]Baba, litukuze jina lako."
Ndipo ikaja sauti kutoka mbinguni,
"Nimelitukuza, nami nitalitukuza tena."
29 [t]Ule umati wa watu uliokuwa mahali
pale uliisikia nao ukasema, "Hiyo ni sauti
ya radi," wengine wakasema, "Malaika
ameongea naye."

---

[a]**12:10** Lk 16:31
[b]**12:11** Yn 11:45; 12:18
[c]**12:12** Mt 21:8; Mk 11:8; Lk 19:35, 36
[d]**12:13** Za 118:25-26; Yn 1:49
[e]13 Kiebrania kusema Okoa, basi likawa neno la shangwe.
[f]**12:14** Mt 21:7
[g]**12:15** Zek 9:9
[h]**12:16** Lk 18:34; Yn 7:39
[i]**12:17** Yn 11:42
[j]**12:18** Yn 12:11; 19:37
[k]**12:19** Yn 11:47, 48
[l]**12:20** Yn 7:35; Mdo 11:20
[m]**12:21** Mt 11:21; Yn 1:44
[n]**12:23** Yn 13:32; 17:1
[o]**12:24** 1Kor 15:36
[p]**12:25** Mk 8:35; Lk 14:26
[q]**12:26** Flp 1:23
[r]**12:27** Mt 26:38, 39; Lk 12:50; Yn 13:21; Lk 22:53; Yn 18:37
[s]**12:28** Mt 3:17
[t]**12:29** Lk 22:43

30 [a]Yesu akawaambia, “Sauti hii imesikika
kwa faida yenu, wala si kwa faida yangu.
31 [b]Sasa ni saa ya hukumu kwa ajili ya
ulimwengu huu, sasa mkuu wa ulimwengu
huu atatupwa nje. 32 [c]Lakini mimi,
nikiinuliwa kutoka nchi, nitawavuta watu
wote waje kwangu.” 33 [d]Yesu aliyasema haya
akionyesha ni kifo gani atakachokufa.

34 [e]Ule umati wa watu ukapiga kelele
ukasema, “Tumesikia kutoka Sheria
kwamba ‘Kristo[f] adumu milele,’ wewe
wawezaje kusema, ‘Mwana wa Adamu
hana budi kuinuliwa juu’? Huyu ‘Mwana
wa Adamu’ ni nani?”

35 [g]Ndipo Yesu akawaambia, “Bado
kitambo kidogo nuru ingalipo pamoja
nanyi. Enendeni maadamu mna nuru,
msije mkakumbwa na giza. Mtu
anayetembea gizani hajui anakokwenda.
36 [h]Wekeni tumaini lenu katika nuru hiyo
ili mpate kuwa wana wa nuru.” Baada ya
kusema haya, Yesu aliondoka, akajificha
wasimwone.

*Wayahudi Waendelea Kutokuamini*

37 [i]Hata baada ya Yesu kufanya miujiza
hii yote mbele yao, bado hawakumwamini.
38 [j]Hili lilikuwa ili kutimiza lile neno la
nabii Isaya lililosema:

“Bwana, ni nani aliyeamini ujumbe
wetu,
na mkono wa Bwana umefunuliwa
kwa nani?”

39 [k]Kwa hivyo hawakuamini, kwa sababu
Isaya anasema mahali pengine:

40 [l]“Amewafanya vipofu,
na kuifanya mioyo yao kuwa
migumu,
ili wasiweze kuona kwa macho yao,
wala kuelewa kwa mioyo yao,
wasije wakageuka nami
nikawaponya.”

41 [m]Isaya alisema haya alipoona utukufu wa
Yesu na kunena habari zake.

42 [n]Lakini wengi miongoni mwa viongozi
wa Wayahudi walimwamini, lakini kwa
sababu ya Mafarisayo hawakukiri waziwazi
kwa maana waliogopa kufukuzwa katika
masinagogi. 43 [o]Wao walipenda sifa za
wanadamu kuliko sifa zitokazo kwa Mungu.

*Amwaminiye Yesu Hatabaki Gizani*

44 [p]Yesu akapaza sauti akasema, “Yeyote
aniaminiye, haniamini mimi peke yangu,
bali yeye aliyenituma. 45 [q]Yeyote anionaye
mimi, amemwona yeye aliyenituma.
46 [r]Mimi nimekuja kama nuru ulimwenguni,
ili kwamba kila mtu aniaminiye asibaki
gizani.

47 [s]“Mimi simhukumu mtu yeyote
anayesikia maneno yangu na asiyatii, kwa
maana sikuja kuuhukumu ulimwengu,
bali kuuokoa. 48 [t]Yuko amhukumuye
yeye anikataaye mimi na kutokuyapokea
maneno yangu, yaani, yale maneno
niliyosema yenyewe yatamhukumu siku
ya mwisho. 49 [u]Kwa maana sisemi kwa ajili
yangu mwenyewe, bali Baba aliyenituma
aliniamuru ni nini cha kusema na jinsi
ya kukisema. 50 [v]Nami ninajua amri zake
huongoza hadi kwenye uzima wa milele.
Hivyo lolote nisemalo, ndilo lile Baba
aliloniambia niseme.”

---

[a]**12:30** Kut 19:9
[b]**12:31** Yn 16; 11; Efe 2:2; 1Yn 5:19
[c]**12:32** Isa 11:10; Yn 3:14; 6:44
[d]**12:33** Yn 18:32; 21:19
[e]**12:34** Za 110:4; Isa 9:7; Mt 8:20; Yn 3:14
[f]34 *Kristo* maana yake ni *Masiya*, yaani *Aliyetiwa mafuta.*
[g]**12:35** Yn 1:9; 8:12; 9:5; Yer 13:16; Efe 5:8; 1Yn 2:11
[h]**12:36** Lk 16:8; Efe 5:8; 1The 5:5; 1Yn 2:9, 10, 11; Yn 8:59; 11:54
[i]**12:37** Yn 2:11
[j]**12:38** Isa 53:1; Rum 10:16
[k]**12:39** Isa 6:9, 10; Mt 13:14, 15
[l]**12:40** Isa 6:10; Mt 13:13, 15
[m]**12:41** Isa 6:1-4; Lk 24:27
[n]**12:42** Yn 7:48; 9:22
[o]**12:43** Yn 5:44; Rum 2:29
[p]**12:44** Mt 10:40; Yn 5:24
[q]**12:45** Yn 14:9
[r]**12:46** Yn 3:19; 8:12
[s]**12:47** Yn 3:17
[t]**12:48** Yn 5:45
[u]**12:49** Yn 14:31
[v]**12:50** Yn 8:26, 28

### *Yesu Awanawisha Wanafunzi Wake Miguu*

13 [a]Ilikuwa mara tu kabla ya Sikukuu ya
Pasaka. Yesu alijua ya kuwa wakati
wake wa kuondoka ulimwenguni ili kurudi
kwa Baba umewadia. Alikuwa amewapenda
watu wake waliokuwa ulimwenguni, naam,
aliwapenda hadi kipimo cha mwisho.
2 [b]Wakati alipokuwa akila chakula cha
jioni na wanafunzi wake, ibilisi alikuwa
amekwisha kutia ndani ya moyo wa Yuda
Iskariote, mwana wa Simoni, wazo la
kumsaliti Yesu. 3 [c]Yesu akijua ya kwamba
Baba ameweka vitu vyote chini ya mamlaka
yake na kwamba yeye alitoka kwa Mungu
na alikuwa anarudi kwa Mungu, 4 [d]hivyo
aliondoka chakulani, akavua vazi lake la
nje, akajifunga kitambaa kiunoni. 5 [e]Kisha
akamimina maji kwenye sinia na kuanza
kuwanawisha wanafunzi wake miguu na
kuikausha kwa kile kitambaa alichokuwa
amejifunga kiunoni.
6 [f]Alipomfikia Simoni Petro, Petro
akamwambia, "Bwana, je, wewe
utaninawisha mimi miguu?"
7 [g]Yesu akamjibu, "Hivi sasa hutambui
lile ninalofanya, lakini baadaye utaelewa."
8 [h]Petro akamwambia, "La, wewe
hutaninawisha miguu kamwe."
Yesu akamjibu, "Kama nisipokunawisha,
wewe huna sehemu nami."
9 Ndipo Simoni Petro akajibu,
"Usininawishe miguu peke yake, Bwana,
bali pamoja na mikono na kichwa pia!"
10 [i]Yesu akamjibu, "Mtu aliyekwisha
kuoga anahitaji kunawa miguu tu, kwani
mwili wake wote ni safi. Ninyi ni safi,
ingawa si kila mmoja wenu." 11 [j]Kwa kuwa
yeye alijua ni nani ambaye angemsaliti,
ndiyo sababu akasema si kila mmoja
aliyekuwa safi.
12 Alipomaliza kuwanawisha miguu yao,
alivaa tena mavazi yake, akarudi alikokuwa
ameketi, akawauliza, "Je, mmeelewa
nililowafanyia? 13 [k]Ninyi mnaniita mimi
'Mwalimu' na 'Bwana,' hii ni sawa, maana
ndivyo nilivyo. 14 [l]Kwa hiyo, ikiwa mimi
niliye Bwana wenu na Mwalimu wenu
nimewanawisha ninyi miguu, pia hamna
budi kunawishana miguu ninyi kwa
ninyi. 15 [m]Mimi nimewawekea kielelezo
kwamba imewapasa kutenda kama vile
nilivyowatendea ninyi. 16 [n]Amin, amin
nawaambia, mtumishi si mkuu kuliko
bwana wake, wala aliyetumwa si mkuu
kuliko yule aliyemtuma. 17 [o]Sasa kwa kuwa
mmejua mambo haya, heri yenu ninyi kama
mkiyatenda.
18 [p]"Sisemi hivi kuhusu ninyi nyote.
Ninawajua wale niliowachagua. Lakini ni
ili Andiko lipate kutimia, kwamba, 'Yeye
aliyekula chakula changu, ameinua kisigino
chake dhidi yangu.'
19 [q]"Ninawaambia mambo haya kabla
hayajatukia, ili yatakapotukia mpate
kuamini ya kuwa Mimi ndiye. 20 [r]Amin,
amin nawaambia, yeyote anayempokea
yule niliyemtuma anipokea mimi, naye
anipokeaye mimi ampokea yeye aliyenituma
mimi."

### *Yesu Anatabiri Kusalitiwa Kwake*

**(Mathayo 26:20-25; Marko 14:17-21; Luka 22:21-23)**

21 [s]Baada ya kusema haya, Yesu
alifadhaika sana moyoni, akasema, "Amin,
amin nawaambia, mmoja wenu atanisaliti."
22 Wanafunzi wake wakatazamana bila
kujua kuwa alikuwa anamsema nani.
23 [t]Mmoja wa wanafunzi wake ambaye Yesu
alimpenda sana, alikuwa ameegama kifuani

---

[a]**13:1** Yn 11:55; 12:33; 16:28
[b]**13:2** Lk 22:3
[c]**13:3** Mt 28:18; Yn 8:42; 17:8
[d]**13:4** Mt 11:29; 20:29; Lk 12:37
[e]**13:5** Lk 7:44
[f]**13:6** 1Pet 5:5
[g]**13:7** Yn 13:12
[h]**13:8** Yn 3:5; 1Kor 6:11; Efe 5:26; Tit 3:5; Ebr 10:22
[i]**13:10** Yn 15:3
[j]**13:11** Mt 10:4
[k]**13:13** Mt 26:18; Yn 11:28; Mdo 10:36
[l]**13:14** 1Pet 5:5
[m]**13:15** Mt 11:29; 1Tim 4:12
[n]**13:16** Mt 10:24; Lk 6:40
[o]**13:17** Lk 11:28; 1:25
[p]**13:18** Za 41:9; Mt 26:23
[q]**13:19** Yn 14:29; 16:4; 4:26; 8:24
[r]**13:20** Mt 10:40; Lk 10:16
[s]**13:21** Yn 12:27; Mt 26:21
[t]**13:23** Yn 20:2; 21:7, 20

mwa Yesu. 24 Simoni Petro akampungia
mkono yule mwanafunzi, akamwambia,
"Muulize anamaanisha nani."
25 [a]Yule mwanafunzi akamwegemea Yesu,
akamuuliza, "Bwana, tuambie, ni nani?"
26 [b]Yesu akajibu, "Ni yule nitakayempa
hiki kipande cha mkate baada ya
kukichovya kwenye bakuli." Hivyo baada
ya kukichovya kile kipande cha mkate,
akampa Yuda Iskariote, mwana wa Simoni.
27 [c]Mara tu baada ya kukipokea kile kipande
cha mkate, Shetani akamwingia.
Yesu akamwambia Yuda, "Lile unalotaka
kulitenda litende haraka." 28 Hakuna hata
mmoja wa wale waliokuwa wameketi
naye mezani aliyeelewa kwa nini Yesu
alimwambia hivyo. 29 [d]Kwa kuwa Yuda
alikuwa mtunza fedha, wengine walifikiri
Yesu alikuwa amemwambia akanunue
vitu vilivyohitajika kwa ajili ya Sikukuu,
au kuwapa maskini chochote. 30 [e]Mara tu
baada ya kupokea ule mkate, Yuda akatoka
nje. Wakati huo ulikuwa ni usiku.

*Yesu Atabiri Petro Kumkana*

**(Mathayo 26:31-35; Marko 14:27-31; Luka 22:31-34)**

31 [f]Baada ya Yuda kutoka nje, Yesu
akasema, "Sasa Mwana wa Adamu
ametukuzwa, naye Mungu ametukuzwa
ndani yake. 32 [g]Ikiwa Mungu ametukuzwa
ndani ya Mwana, Mungu atamtukuza
Mwana ndani yake mwenyewe naye
atamtukuza mara.
33 [h]"Watoto wangu, mimi bado niko
pamoja nanyi kwa kitambo kidogo.
Mtanitafuta, na kama vile nilivyowaambia
Wayahudi, vivyo hivyo sasa nawaambia na
ninyi. Niendako, ninyi hamwezi kuja.
34 [i]"Amri mpya nawapa: Mpendane kama
mimi nilivyowapenda ninyi, vivyo hivyo
nanyi mpendane. 35 [j]Kama mkipendana
ninyi kwa ninyi, kwa njia hii, watu wote
watajua kuwa ninyi ni wanafunzi wangu."
36 [k]Simoni Petro akamuuliza, "Bwana,
unakwenda wapi?"
Yesu akamjibu, "Ninakokwenda huwezi
kunifuata sasa, lakini utanifuata baadaye."
37 [l]Petro akamuuliza tena, "Bwana, kwa
nini siwezi kukufuata sasa? Mimi niko
tayari kuutoa uhai wangu kwa ajili yako."
38 [m]Yesu akamjibu, "Je, ni kweli uko tayari
kuutoa uhai wako kwa ajili yangu? Amin,
amin nakuambia, kabla jogoo hajawika,
utanikana mara tatu."

*Yesu Awatia Moyo Wanafunzi Wake*

14 [n]Yesu akawaambia, "Msifadhaike
mioyoni mwenu, mnamwamini
Mungu, niaminini na mimi pia. 2 [o]Nyumbani
kwa Baba yangu kuna makao mengi.
Kama sivyo, ningeliwaambia. Naenda
kuwaandalia makao. 3 [p]Nami nikienda
na kuwaandalia makao, nitarudi tena na
kuwachukua mkae pamoja nami, ili mahali
nilipo, nanyi mpate kuwepo. 4 Ninyi mnajua
njia ya kufika ninakokwenda."

*Yesu Ndiye Njia Ya Kwenda Kwa Baba*

5 [q]Tomaso akamwambia, "Bwana, sisi
hatujui unakokwenda, tutaijuaje njia?"
6 [r]Yesu akawaambia, "Mimi ndimi njia na
kweli na uzima. Mtu hawezi kuja kwa Baba
isipokuwa kwa kupitia kwangu. 7 [s]Kama
mngenijua mimi, mngemjua na Baba pia.
Tangu sasa, mnamjua Baba yangu, tena
mmemwona."

---

[a]**13:25** Mt 26:22; Yn 21:20
[b]**13:26** Mt 10:4
[c]**13:27** Lk 22:3
[d]**13:29** Yn 12:6
[e]**13:30** Lk 22:53
[f]**13:31** Yn 7:39; 12:23; 17:4; 1Pet 4:11
[g]**13:32** Yn 17:1
[h]**13:33** Yn 7:33, 34
[i]**13:34** 1Yn 2:7-11; 3:11; Law 19:18; 1The 4:9; Efe 5:2; 1Yn 4:10, 11; 2:14
[j]**13:35** Yn 3:14; 4:20
[k]**13:36** Yn 16:5; 14:2; 21:18, 19; 2Pet 1:4
[l]**13:37** Mt 26:33, 34, 35; Mk 14:29, 30, 31; Lk 22:33, 34
[m]**13:38** Yn 18:27
[n]**14:1** Yn 14:27; 3:19; Za 4:5; Mk 11:22
[o]**14:2** Yn 13:33, 36; 16:5
[p]**14:3** Yn 12:26
[q]**14:5** Yn 11:16
[r]**14:6** Efe 2:18; Ebr 10:20; Yn 1:25; Mdo 4:12
[s]**14:7** Yn 8:19; 1Yn 2:23

8 [a]Filipo akamwambia, “Bwana,
tuonyeshe Baba yako yatosha.”
9 [b]Yesu akamjibu, “Filipo, nimekaa nanyi
muda huu wote hata usinijue? Mtu yeyote
aliyeniona mimi, amemwona Baba. Sasa
wawezaje kusema, ‘Tuonyeshe Baba’?
10 [c]Je, huamini ya kuwa mimi niko ndani
ya Baba, naye Baba yuko ndani yangu?
Maneno ninayowaambia siyasemi kwa ajili
yangu mwenyewe, bali Baba akaaye ndani
yangu ndiye atendaye hizi kazi. 11 [d]Nisadiki
mimi kwamba niko ndani ya Baba na Baba
yuko ndani yangu, la sivyo, niaminini kwa
sababu ya zile kazi nizitendazo. 12 [e]Amin,
amin nawaambia, yeyote aniaminiye
mimi, kazi nizifanyazo yeye atazifanya,
naam na kubwa kuliko hizi atazifanya,
kwa sababu mimi ninakwenda kwa Baba.
13 [f]Nanyi mkiomba lolote kwa Jina langu,
hilo nitalifanya, ili Baba apate kutukuzwa
katika Mwana. 14 Kama mkiniomba lolote
kwa Jina langu nitalifanya.

### *Yesu Aahidi Roho Mtakatifu*

15 [g]“Kama mnanipenda, mtazishika amri
zangu. 16 [h]Nami nitamwomba Baba, naye
atawapa Msaidizi mwingine akae nanyi
milele. 17 [i]Huyo ndiye Roho wa kweli
ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea,
kwa sababu haumwoni wala haumjui. Ninyi
mnamjua kwa kuwa yuko pamoja nanyi
naye anakaa ndani yenu. 18 [j]Sitawaacha
ninyi yatima, naja kwenu. 19 [k]Bado kitambo
kidogo ulimwengu hautaniona tena, ila
ninyi mtaniona, kwa kuwa mimi ni hai,
ninyi nanyi mtakuwa hai. 20 [l]Wakati huo
mtajua ya kuwa mimi niko ndani ya Baba
na ninyi mko ndani yangu na mimi niko
ndani yenu. 21 [m]Yeyote mwenye amri zangu
na kuzishika ndiye anipendaye, naye
anipendaye atapendwa na Baba yangu,
nami nitampenda na kujidhihirisha kwake.”
22 [n]Ndipo Yuda, siyo Iskariote,
akamwambia, “Bwana, itakuwaje
kwamba utajidhihirisha kwetu na si kwa
ulimwengu?”
23 [o]Yesu akamjibu, “Mtu yeyote
akinipenda atalishika neno langu na Baba
yangu atampenda, nasi tutakuja kwake na
kufanya makao yetu kwake. 24 [p]Mtu yeyote
asiyenipenda hayashiki maneno yangu na
maneno niliyowapa si yangu bali ni ya Baba
aliyenituma.
25 “Nimewaambia mambo haya yote
wakati bado niko pamoja nanyi. 26 [q]Lakini
huyo Msaidizi, yaani, huyo Roho Mtakatifu,
ambaye Baba atamtuma kwenu kwa Jina
langu, atawafundisha mambo yote na
kuwakumbusha yote niliyowaambia.
27 [r]Amani nawaachia, amani yangu nawapa,
amani hii niwapayo si kama ile ulimwengu
utoayo. Msifadhaike mioyoni mwenu, wala
msiogope.
28 [s]“Mlinisikia nikisema, ‘Ninakwenda
zangu, lakini nitarudi tena.’ Kama kweli
mngelinipenda mngelifurahi kwa kuwa
naenda kwa Baba, kwani Baba ni mkuu
kuniliko mimi. 29 [t]Nimewaambia mambo
haya kabla hayajatukia, ili yatakapotukia
mpate kuamini. 30 [u]Sitasema nanyi zaidi,
kwa sababu yule mkuu wa ulimwengu
huu anakuja, naye hana kitu kwangu,
31 [v]lakini ulimwengu upate kujua kuwa
ninampenda Baba, nami hufanya vile Baba
alivyoniamuru.
“Haya inukeni; twendeni zetu.

---

[a]**14:8** Yn 1:43
[b]**14:9** Isa 9:6; Kol 1:15
[c]**14:10** Yn 14:20; 10:38; 17:21, 23; 5:19; 7:16
[d]**14:11** Yn 5:36; 10:38
[e]**14:12** Mt 21:21; Lk 10:17
[f]**14:13** Mt 7:7
[g]**14:15** Za 103:18
[h]**14:16** Yn 15:26; 16:7
[i]**14:17** 1Yn 4:6; 5:6; 1Kor 2:14
[j]**14:18** Mt 16:27
[k]**14:19** Yn 7:33, 34; 16:16; 6:57
[l]**14:20** Yn 17:21
[m]**14:21** Yn 14:15; Kum 7:13; Yn 16:27
[n]**14:22** Lk 6:16; Mdo 1:13; 10:41
[o]**14:23** Rum 8:10; Yn 14:15
[p]**14:24** Yn 5:19
[q]**14:26** Yn 15:26; 16:7; Mdo 2:33; Yn 16:13; 2:22; 1Yn 2:20, 27
[r]**14:27** Hes 6:26; Lk 2:14
[s]**14:28** Mt 16:27; Yn 5:18; 10:29; Flp 2:6
[t]**14:29** Yn 13:19; 16:4
[u]**14:30** Yn 12:31
[v]**14:31** Yn 10:18; 12:49

*Yesu Mzabibu Wa Kweli*

15 [a]"Mimi ndimi mzabibu wa kweli na
Baba yangu ndiye mkulima. 2 [b]Kila
tawi ndani yangu lisilozaa matunda, Baba
yangu hulikata, nalo kila tawi lizaalo,
hulisafisha ili lipate kuzaa matunda zaidi.
3 [c]Ninyi mmekwisha kuwa safi kwa sababu
ya lile neno nililonena nanyi. 4 [d]Kaeni ndani
yangu, nami nikae ndani yenu. Kama vile
tawi lisivyoweza kuzaa matunda lisipokaa
ndani ya mzabibu, vivyo hivyo ninyi
msipokaa ndani yangu hamwezi kuzaa
matunda.
5 [e]"Mimi ni mzabibu, ninyi ni matawi.
Akaaye ndani yangu, nami ndani yake,
huyo huzaa sana, maana pasipo mimi ninyi
hamwezi kufanya jambo lolote. 6 [f]Mtu
yeyote asipokaa ndani yangu, hutupwa
nje kama tawi na kunyauka. Matawi kama
hayo hukusanywa na kutupwa motoni,
yakateketea. 7 [g]Ninyi mkikaa ndani yangu
na maneno yangu yakikaa ndani yenu,
ombeni lolote mtakalo, nanyi mtatendewa.
8 [h]Kwa hiyo Baba yangu hutukuzwa, kwa
vile mzaavyo matunda mengi, nanyi
mtakuwa wanafunzi wangu.
9 [i]"Kama vile Baba alivyonipenda mimi,
hivyo ndivyo mimi nilivyowapenda ninyi.
Basi kaeni katika pendo langu. 10 [j]Mkizishika
amri zangu mtakaa katika pendo langu, kama
mimi nilivyozishika amri za Baba yangu na
kukaa katika pendo lake. 11 [k]Nimewaambia
mambo haya ili furaha yangu iwe ndani
yenu na furaha yenu iwe kamili. 12 [l]Amri
yangu ndiyo hii: Mpendane kama mimi
nilivyowapenda ninyi. 13 [m]Hakuna mtu
mwenye upendo mkuu kuliko huu, mtu
kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki
zake. 14 [n]Ninyi ni rafiki zangu mkifanya
ninayowaamuru. 15 [o]Siwaiti ninyi watumishi
tena, kwa sababu watumishi hawajui
bwana wao analofanya, bali nimewaita
ninyi rafiki, kwa maana nimewajulisha
mambo yote niliyoyasikia kutoka kwa
Baba yangu. 16 [p]Si ninyi mlionichagua,
bali mimi ndiye niliyewachagua ninyi na
kuwaweka mwende mkazae matunda, na
matunda yenu yapate kudumu. Ili nalo
lolote mtakalomwomba Baba katika Jina
langu, awape ninyi. 17 [q]Amri yangu ndiyo
hii: Mpendane.

*Ulimwengu Wawachukia Wanafunzi*

18 [r]"Kama ulimwengu ukiwachukia
ninyi, kumbukeni kwamba ulinichukia
mimi kabla yenu. 19 [s]Kama mngekuwa wa
ulimwengu, ulimwengu ungeliwapenda
kama vile unavyowapenda walio wake.
Kwa sababu ninyi si wa ulimwengu, lakini
mimi nimewachagua kutoka ulimwenguni,
hii ndiyo sababu ulimwengu unawachukia.
20 [t]Kumbukeni lile neno nililowaambia,
'Hakuna mtumishi aliye mkuu kuliko
bwana wake.' Kama wamenitesa mimi,
nanyi pia watawatesa. Kama walilishika
neno langu, watalishika na neno lenu pia.
21 [u]Watawatendea ninyi haya yote kwa ajili
ya Jina langu, kwa sababu hawamjui yeye
aliyenituma. 22 [v]Kama sikuja na kusema
nao wasingalikuwa na hatia ya dhambi.
Lakini sasa hawana udhuru kwa ajili ya
dhambi zao. 23 [w]Yeyote anayenichukia
mimi, anamchukia pia na Baba yangu.
24 [x]Kama sikuwa nimefanya miujiza
ambayo haijapata kufanywa na mtu
mwingine yeyote, wasingalikuwa na hatia

[a]**15:1** Za 80:8-11
[b]**15:2** Mt 3:10; Za 92:14; Mt 3:8; 7:20; Gal 5:22; Efe 5:9; Flp 1:11; Yn 16:6
[c]**15:3** Yn 17:17; Efe 5:26
[d]**15:4** Yn 6:56; 2:6
[e]**15:5** 1Kor 12:12, 27; 2Kor 3:5
[f]**15:6** Mt 3:10; 13:40; Eze 15:4; Yn 15:2
[g]**15:7** Mk 11:24; Yn 6:56; Mt 7:7
[h]**15:8** Mt 5:16; Yn 8:31
[i]**15:9** Yn 17:23, 24, 26
[j]**15:10** Yn 14:15
[k]**15:11** Yn 3:29
[l]**15:12** Yn 13:34; 1Yn 3:11; Mk 12:30
[m]**15:13** Mwa 44:33; Rum 5:7, 8
[n]**15:14** Mit 18:24; Mt 12:50
[o]**15:15** Yn 8:26
[p]**15:16** Yn 6:70; 13:18
[q]**15:17** Yn 15:12
[r]**15:18** Isa 66:5
[s]**15:19** Yn 15:16; 17:14
[t]**15:20** Yn 13:16; 2Tim 3:12
[u]**15:21** Isa 66:5; Yn 16:3
[v]**15:22** Rum 1:20; 2:1
[w]**15:23** 1Yn 2:23
[x]**15:24** Yn 5:36

ya dhambi. Lakini sasa wameiona miujiza
hii na bado wakatuchukia mimi na Baba
yangu. 25 [a]Lakini hii ni kutimiza lile neno
lililoandikwa kwenye Sheria kwamba,
‘Walinichukia pasipo sababu.’
26 [b]“Lakini atakapokuja huyo Msaidizi
nitakayemtuma kwenu kutoka kwa Baba,
yaani, huyo Roho wa kweli atokaye kwa
Baba, yeye atanishuhudia mimi. 27 [c]Ninyi
nanyi itawapasa kushuhudia kwa sababu
mmekuwa pamoja nami tangu mwanzo.

16 [d]“Nimewaambia mambo haya yote ili
msije mkaiacha imani. 2 [e]Watawatenga
na masinagogi. Naam, saa yaja ambayo
mtu yeyote atakayewaua atadhani kwa
kufanya hivyo anamtumikia Mungu. 3 [f]Nao
watawatenda haya kwa sababu hawamjui
Baba wala mimi. 4 [g]Lakini nimewaambia
ninyi mambo haya, ili saa hiyo ikiwadia
mpate kukumbuka ya kuwa nilikuwa
nimewaambia. Sikuwaambia mambo
haya tangu mwanzo kwa sababu nilikuwa
pamoja nanyi.

*Kazi Ya Roho Mtakatifu*

5 [h]“Sasa mimi ninakwenda kwake
yeye aliyenituma, lakini hakuna hata
aniulizaye, ‘Unakwenda wapi?’ 6 [i]Kwa
sababu nimewaambia mambo haya,
mioyo yenu imejawa na huzuni. 7 [j]Lakini
nawaambia kweli, yafaa mimi niondoke,
kwa kuwa nisipoondoka, huyo Msaidizi
hatakuja kwenu, lakini nikienda nitamtuma
kwenu. 8 [k]Naye atakapokuja, atauthibitishia
ulimwengu kuhusu dhambi, haki na
hukumu. 9 [l]Kwa habari ya dhambi, kwa
sababu hawaniamini mimi, 10 [m]kwa habari
ya haki, kwa sababu ninakwenda kwa Baba,
nanyi hamtaniona tena, 11 [n]kwa habari
ya hukumu, kwa sababu yule mkuu wa
ulimwengu huu amekwisha kuhukumiwa.
12 [o]“Bado ninayo mambo mengi ya
kuwaambia, lakini hamwezi kuyastahimili
sasa. 13 [p]Atakapokuja huyo Roho wa
kweli atawaongoza awatie katika kweli
yote. Yeye hatanena kwa ajili yake
mwenyewe, bali atanena yale yote
atakayosikia, naye atawaonyesha mambo
yajayo. 14 Atanitukuza mimi, kwa maana
atayachukua yaliyo yangu na kuwajulisha
ninyi. 15 [q]Vyote alivyo navyo Baba ni vyangu.
Ndiyo maana nimesema Roho atachukua
yaliyo yangu na kuwajulisha ninyi.
16 [r]“Bado kitambo kidogo nanyi
hamtaniona na tena bado kitambo kidogo
nanyi mtaniona.”

*Huzuni Itageuka Kuwa Furaha*

17 [s]Baadhi ya wanafunzi wakaulizana,
“Ana maana gani asemapo, ‘Bado kitambo
kidogo nanyi hamtaniona na tena bado
kitambo kidogo nanyi mtaniona’? Naye
ana maana gani asemapo, ‘Kwa sababu
ninakwenda kwa Baba’?” 18 Wakaendelea
kuulizana, “Ana maana gani asemapo,
‘Kitambo kidogo’? Hatuelewi hilo
analosema.”
19 Yesu akatambua kuwa walitaka
kumuuliza juu ya hilo, hivyo akawaambia,
“Je, mnaulizana nina maana gani
niliposema, ‘Bado kitambo kidogo nanyi
hamtaniona na tena bado kitambo
kidogo nanyi mtaniona’? 20 [t]Amin, amin
nawaambia, ninyi mtalia na kuomboleza,
lakini ulimwengu utafurahi. Ninyi
mtahuzunika, lakini huzuni yenu itageuka
kuwa furaha. 21 [u]Mwanamke anapokuwa na
utungu wa kuzaa huwa na maumivu kwa
sababu saa yake imewadia. Lakini mtoto
akiisha kuzaliwa, yule mwanamke husahau

[a]**15:25** Za 69:4; 109:3
[b]**15:26** Yn 14:15; 16:7; 14:17; 1Yn 4:4
[c]**15:27** Lk 24:48; 1:21; 1Yn 4:14
[d]**16:1** Yn 15:18-27; Mt 11:16
[e]**16:2** Yn 12:42; Isa 66:5; Ufu 6:9
[f]**16:3** Yn 17:25; 1Yn 3:1
[g]**16:4** Yn 14:29
[h]**16:5** Yn 16:10, 17, 28; 7:33; 13:36; 14:5
[i]**16:6** Yn 6:22; 14:1
[j]**16:7** Yn 14:16, 26; 15:26
[k]**16:8** 1Kor 14:24; Ebr 4:12
[l]**16:9** Yn 15:22
[m]**16:10** Rum 1:17; 1Pet 3:18
[n]**16:11** Yn 12:31
[o]**16:12** 1Kor 3:2
[p]**16:13** Yn 14:17; Za 25:5
[q]**16:15** Yn 17:10
[r]**16:16** Yn 7:33; 16:22; 14:18-24
[s]**16:17** Yn 16:16; 16:5
[t]**16:20** Mk 16:10; Yn 20:20
[u]**16:21** Mik 4:9; 1The 5:3

maumivu hayo kwa sababu ya furaha ya
kuzaliwa mtoto ulimwenguni. 22 [a]Hivyo
ninyi mna maumivu sasa, lakini nitawaona
tena, nayo mioyo yenu itafurahi na furaha
yenu hakuna awaondoleaye. 23 [b]Katika
siku hiyo hamtaniuliza neno lolote. Amin,
amin nawaambia, kama mkimwomba Baba
jambo lolote kwa jina langu, yeye atawapa.
24 [c]Mpaka sasa hamjaomba jambo lolote
kwa Jina langu. Ombeni nanyi mtapewa,
ili furaha yenu ipate kuwa kamili.

*Amani Kwa Wanafunzi*

25 [d]"Nimewaambia mambo haya kwa
mafumbo. Saa yaja ambapo sitazungumza
nanyi tena kwa mafumbo bali nitawaeleza
waziwazi kuhusu Baba. 26 [e]Siku hiyo
mtaomba kwa Jina langu. Wala sitawaambia
kwamba nitamwomba Baba kwa ajili
yenu, 27 [f]kwa maana Baba mwenyewe
anawapenda, kwa sababu mmenipenda
mimi na mmeamini kwamba nimetoka
kwa Mungu. 28 [g]Nilitoka kwa Baba na kuja
ulimwenguni, sasa naondoka ulimwenguni
na kurudi kwa Baba."

29 [h]Ndipo wanafunzi wake wakasema,
"Sasa unazungumza waziwazi, wala si kwa
mafumbo. 30 [i]Sasa tumejua kwamba wewe
unajua mambo yote, wala hakuna haja ya
mtu kukuuliza maswali. Kwa jambo hili
tunaamini kwamba ulitoka kwa Mungu."

31 Yesu akawajibu, "Je, sasa mnaamini?
32 [j]Saa inakuja, naam, imekwisha kuwadia,
mtakapotawanyika kila mmoja kwenda
nyumbani kwake na kuniacha peke yangu.
Lakini mimi siko peke yangu kwa sababu
Baba yu pamoja nami. 33 [k]Nimewaambia
mambo haya, ili mpate kuwa na amani
mkiwa ndani yangu. Ulimwenguni mtapata
dhiki. Lakini jipeni moyo, kwa maana mimi
nimeushinda ulimwengu."

*Yesu Ajiombea Mwenyewe*

17 [l]Baada ya Yesu kusema haya, alitazama
kuelekea mbinguni akawaombea na
kusema:

"Baba, saa imewadia. Umtukuze
Mwanao, ili Mwanao apate kukutukuza
wewe. 2 [m]Kwa kuwa umempa mamlaka
juu ya wote wenye mwili ili awape
uzima wa milele wale uliompa. 3 [n]Nao
uzima wa milele ndio huu, wakujue
wewe uliye Mungu wa pekee, wa
kweli na Yesu Kristo uliyemtuma.
4 [o]Nimekutukuza wewe duniani kwa
kuitimiza ile kazi uliyonipa niifanye.
5 [p]Hivyo sasa, Baba, unitukuze mbele
zako kwa ule utukufu niliokuwa nao
pamoja na wewe kabla ulimwengu
haujakuwepo.

*Yesu Awaombea Wanafunzi Wake*

6 [q]"Nimelidhihirisha jina lako kwa
wale ulionipa kutoka ulimwengu.
Walikuwa wako, nawe ukanipa
mimi, nao wamelitii neno lako. 7 Sasa
wamejua ya kuwa vyote ulivyonipa
vimetoka kwako, 8 [r]kwa kuwa maneno
yale ulionipa nimewapa wao, nao
wameyapokea na kujua kwamba kweli
nimetoka kwako, nao wameamini kuwa
wewe ulinituma. 9 [s]Ninawaombea
wao. Mimi siuombei ulimwengu,
bali nawaombea wale ulionipa kwa
sababu wao ni wako. 10 [t]Wote walio
wangu ni wako na walio wako ni
wangu, nami nimetukuzwa ndani yao.

[a]**16:22** Isa 60:14; Lk 24:41, 52; Yn 14:1, 27; Mdo 2:46; 13:52; 1Pet 1:8
[b]**16:23** Mt 7:7; Yn 15:16
[c]**16:24** Yn 3:29; 15:11
[d]**16:25** Yn 10:6
[e]**16:26** Yn 16:23, 24
[f]**16:27** Yn 14:21, 23
[g]**16:28** Yn 5:10, 17; 13:3
[h]**16:29** Yn 16:25
[i]**16:30** 1Fal 17:24; Yn 16:27; 13:3; 2:25
[j]**16:32** Yn 16:2, 25; Mt 26:31; 26:56; Yn 8:16, 29
[k]**16:33** Yn 14:27; 15:18-21; 1Yn 5:4; Ufu 21:7
[l]**17:1** Yn 11:41; 12:23; 13:31, 32
[m]**17:2** Dan 7:14; Yn 6:37, 39
[n]**17:3** Flp 3:8; Yn 17:8, 18, 21, 23, 25; 3:17
[o]**17:4** Yn 13:31; 19:30
[p]**17:5** Flp 2:6; Yn 1:2
[q]**17:6** Yn 17:26; 1:18
[r]**17:8** Yn 8:26; 1:18
[s]**17:9** Lk 22:32
[t]**17:10** Yn 16:15

11 [a]Mimi sasa simo tena ulimwenguni,
lakini wao bado wamo ulimwenguni,
nami naja kwako. Baba Mtakatifu,
uwalinde kwa uweza wa jina lako
ulilonipa, ili wawe na umoja kama
sisi tulivyo wamoja. 12 [b]Nilipokuwa
pamoja nao, niliwalinda, wakawa
salama kwa lile jina ulilonipa. Hakuna
hata mmoja aliyepotea, isipokuwa yule
aliyekusudiwa upotevu, ili Maandiko
yapate kutimia.
13 [c]"Lakini sasa naja kwako, nami
ninasema mambo haya wakati
bado nikiwa ulimwenguni, ili wawe
na furaha yangu kamili ndani
yao. 14 [d]Nimewapa neno lako, nao
ulimwengu umewachukia kwa kuwa
wao si wa ulimwengu kama mimi
nisivyo wa ulimwengu huu. 15 [e]Siombi
kwamba uwaondoe ulimwenguni, bali
uwalinde dhidi ya yule mwovu. 16 [f]Wao
si wa ulimwengu huu, kama vile mimi
nisivyo wa ulimwengu. 17 [g]Uwatakase
kwa ile kweli, neno lako ndilo kweli.
18 [h]Kama vile ulivyonituma mimi
ulimwenguni, nami nawatuma vivyo
hivyo. 19 [i]Kwa ajili yao najiweka wakfu
ili wao nao wapate kutakaswa katika
ile kweli.

*Yesu Awaombea Wote Wamwaminio*

20 [j]"Siwaombei hawa peke yao,
bali nawaombea na wale wote
watakaoniamini kupitia neno lao 21 [k]ili
wawe na umoja kama vile wewe Baba
ulivyo ndani yangu na mimi nilivyo
ndani yako, wao nao wawe ndani
yetu, ili ulimwengu upate kuamini
ya kuwa wewe ndiye uliyenituma
mimi. 22 [l]Utukufu ule ulionipa
nimewapa wao, ili wawe na umoja
kama sisi tulivyo wamoja. 23 [m]Mimi
ndani yako na wewe ndani yangu, ili
wawe wamekamilika katika umoja
na ulimwengu upate kujua ya kuwa
umenituma, nami nimewapenda wao
kama unavyonipenda mimi.
24 [n]"Baba, shauku yangu ni kwamba,
wale ulionipa wawe pamoja nami pale
nilipo, ili waweze kuuona utukufu
wangu, yaani, utukufu ule ulionipa
kwa kuwa ulinipenda hata kabla ya
kuwekwa misingi ya ulimwengu.
25 [o]"Baba Mwenye Haki, ingawa
ulimwengu haukujui, mimi ninakujua,
nao wanajua ya kuwa umenituma.
26 Nimefanya jina lako lijulikane kwao
nami nitaendelea kufanya lijulikane, ili
kwamba upendo ule unaonipenda mimi
uwe ndani yao na mimi mwenyewe
nipate kuwa ndani yao."

*Yesu Akamatwa*

**(Mathayo 26:47-56; Marko 14:43-50; Luka 22:47-53)**

18 [p]Yesu alipomaliza kuomba, akaondoka
na wanafunzi wake wakavuka Bonde
la Kidroni. Upande wa pili palikuwa na
bustani, yeye na wanafunzi wake wakaingia
humo.
2 [q]Basi Yuda, yule aliyemsaliti alipafahamu
mahali hapo kwani Yesu alikuwa akikutana
humo na wanafunzi wake mara kwa mara.
3 [r]Hivyo Yuda akaja bustanini. Aliongoza
kikosi cha askari wa Kirumi, na baadhi ya
maafisa kutoka kwa viongozi wa makuhani
na Mafarisayo. Nao walikuwa wamechukua
taa, mienge na silaha.
4 [s]Yesu akijua yale yote yatakayompata,

[a]**17:11** Yn 13:1; 17:13; 7:33; 17:21-23; Za 133:1; Yn 10:30
[b]**17:12** Yn 6:39; 6:70
[c]**17:13** Yn 3:29
[d]**17:14** Yn 15:19; 8:23; 1Yn 3:13; Yn 17:16
[e]**17:15** Mt 5:37
[f]**17:16** Yn 17:14
[g]**17:17** 2Sam 7:28; Yn 15:3; 1Fal 17:24
[h]**17:18** Yn 17:3, 8, 21, 23, 25; 20:21
[i]**17:19** Yn 17:17; 1Kor 1:2, 30; 1The 4:7; Ebr 10:10
[j]**17:20** Yn 17:9
[k]**17:21** Gal 3:28; Rum 12:5; Yn 10:38; 14:11
[l]**17:22** Yn 14:20; 1Yn 1:2; 3:24
[m]**17:23** Yn 3:17; 16:27; Kol 3:14
[n]**17:24** Yn 12:26; 1:14; Mt 25:34; Yn 1:2
[o]**17:25** Yn 15:21; 16:3; 3:17; 7:29
[p]**18:1** 2Sam 15:23; Mt 21:1; 26:36
[q]**18:2** Lk 21:37; 22:39
[r]**18:3** Mt 26:47; Mk 14:43; Lk 22:47; Mdo 1:16
[s]**18:4** Yn 6:64; 13:1; 11; 19:28

akajitokeza mbele yao akawauliza,
"Mnamtafuta nani?"
5 [a]Wao wakamjibu, "Yesu wa Nazareti."
Yesu akawajibu, "Mimi ndiye." Yuda,
yule aliyemsaliti alikuwa amesimama
pamoja nao. 6 Yesu alipowaambia, "Mimi
ndiye," walirudi nyuma na kuanguka chini!
7 [b]Akawauliza tena, "Mnamtafuta nani?"
Nao wakamjibu, "Yesu wa Nazareti."
8 Yesu akawaambia, "Nimekwisha
kuwaambia kuwa, mimi ndiye; kwa hiyo
kama mnanitafuta mimi, waacheni hawa
watu waende zao." 9 [c]Hii ilikuwa ili litimie
lile neno alilosema, "Sikumpoteza hata
mmoja miongoni mwa wale ulionipa."
10 [d]Simoni Petro, aliyekuwa na upanga,
akaufuta na kumkata sikio la kuume
mtumishi wa kuhani mkuu. Jina la
mtumishi huyo aliitwa Malko.
11 [e]Yesu akamwambia Petro, "Rudisha
upanga wako kwenye ala yake. Je, hainipasi
kukinywea kikombe alichonipa Baba?"

*Yesu Mbele Ya Kuhani Mkuu*

12 [f]Hivyo wale askari, wakiwa pamoja
na majemadari wao na maafisa wa
Wayahudi, wakamkamata Yesu na
kumfunga. 13 [g]Kwanza wakampeleka kwa
Anasi, mkwewe Kayafa, aliyekuwa kuhani
mkuu mwaka ule. 14 [h]Kayafa ndiye alikuwa
amewashauri Wayahudi kwamba imempasa
mtu mmoja kufa kwa ajili ya watu.

*Petro Anamkana Yesu*

**(Mathayo 26:69-70; Marko 14:55-64; Luka 22:66-71)**

15 [i]Simoni Petro pamoja na mwanafunzi
mwingine walikuwa wakimfuata Yesu.
Huyu mwanafunzi mwingine alikuwa
anafahamika kwa kuhani mkuu, hivyo
aliingia ndani ya ukumbi pamoja na Yesu.
16 [j]Lakini Petro alisimama nje karibu na
lango, ndipo yule mwanafunzi mwingine,
aliyejulikana na kuhani mkuu, akazungumza
na msichana aliyekuwa analinda lango,
akamruhusu Petro aingie ndani.
17 [k]Yule msichana akamuuliza Petro, "Je,
wewe pia si mmoja wa wanafunzi wa mtu
huyu?"
Petro akajibu, "Sio mimi."
18 [l]Wale watumishi na askari walikuwa
wamesimama wakiota moto wa makaa
kwa sababu palikuwa na baridi, Petro naye
alikuwa amesimama pamoja nao akiota
moto.

*Kuhani Mkuu Amhoji Yesu*

19 Wakati huo kuhani mkuu akawa
anamuuliza Yesu kuhusu wanafunzi wake
na mafundisho yake.
20 [m]Yesu akamjibu, "Nimekuwa
nikizungumza waziwazi mbele ya watu
wote. Siku zote nimefundisha katika
masinagogi na Hekaluni, mahali ambapo
Wayahudi wote hukusanyika. Sikusema
jambo lolote kwa siri. 21 Mbona unaniuliza
mimi maswali? Waulize wale walionisikia
yale niliyowaambia. Wao wanajua
niliyosema."
22 [n]Alipomaliza kusema hayo, mmoja wa
askari aliyekuwa amesimama karibu naye,
akampiga Yesu kofi usoni, kisha akasema,
"Je, hivyo ndivyo unavyomjibu kuhani
mkuu?"
23 [o]Yesu akamjibu akasema, "Kama
nimesema jambo baya, shuhudia huo ubaya
niliousema. Lakini kama nimesema yaliyo
kweli, mbona umenipiga?" 24 [p]Ndipo Anasi
akampeleka Yesu kwa kuhani mkuu Kayafa,
akiwa bado amefungwa.

---

[a]**18:5** Mk 1:4
[b]**18:7** Yn 18:4
[c]**18:9** Yn 6:39; 17:12
[d]**18:10** Mt 26:51; Mk 14:47; Lk 22:49, 50
[e]**18:11** Mt 20:22
[f]**18:12** Yn 18:3
[g]**18:13** Yn 18:24; Mt 26:3
[h]**18:14** Yn 11:49-51
[i]**18:15** Mt 26:3; 26:58; Mk 14:54
[j]**18:16** Mt 26:69; Mk 14:66; Lk 22:54
[k]**18:17** Yn 17:25
[l]**18:18** Yn 21:9; Mk 14:54, 67
[m]**18:20** Mt 4:23; 26:55; Yn 7:26
[n]**18:22** Yer 20:2; Mdo 23:2; Mt 16:21
[o]**18:23** Mt 5:39; Mdo 26:3
[p]**18:24** Yn 18:13; Mt 26:3

*Petro Amkana Yesu Tena*

**(Mathayo 26:71-75; Marko 14:69-
72; Luka 22:58-62)**

25 [a]Wakati huo Simoni Petro alikuwa
amesimama akiota moto. Baadhi ya wale
waliokuwepo wakamuuliza, “Je, wewe si
mmoja wa wanafunzi wake?”
Petro akakana, akasema, “Sio mimi.”
26 [b]Mmoja wa watumishi wa kuhani
mkuu, ndugu yake yule mtu ambaye Petro
alikuwa amemkata sikio, akamuuliza, “Je,
mimi sikukuona kule bustanini ukiwa na
Yesu?” 27 [c]Kwa mara nyingine tena Petro
akakana, naye jogoo akawika wakati huo
huo.

*Yesu Apelekwa Kwa Pilato*

**(Mathayo 27:1-2, 11-14; Marko
15:1-5; Luka 23:1-5)**

28 [d]Ndipo Wayahudi wakamchukua Yesu
kutoka kwa Kayafa na kumpeleka kwenye
jumba la kifalme la mtawala wa Kirumi.[e]
Wakati huo ilikuwa ni alfajiri, ili kuepuka
kuwa najisi kwa taratibu za ibada, Wayahudi
hawakuingia ndani kwa sababu ya sheria
za Kiyahudi. Wangehesabiwa kuwa najisi
kama wangeingia nyumbani mwa mtu asiye
Myahudi na wasingeruhusiwa kushiriki
katika Sikukuu ya Pasaka. 29 Hivyo Pilato
akatoka nje walikokuwa akawauliza,
“Mmeleta mashtaka gani kumhusu mtu
huyu?”
30 Wao wakamjibu, “Kama huyu mtu
hakuwa mhalifu tusingemleta kwako.”
31 Pilato akawaambia, “Basi mchukueni
ninyi mkamhukumu kwa kufuata sheria
zenu.”
Wayahudi wakamjibu, “Sisi haturuhusiwi
kutoa hukumu ya kifo kwa mtu yeyote.”
32 [f]Walisema hivyo ili yale maneno
aliyosema Yesu kuhusu kifo atakachokufa
yapate kutimia.

33 [g]Kwa hiyo Pilato akaingia ndani
ya jumba la kifalme, akamwita Yesu,
akamuuliza, “Wewe ndiye mfalme wa
Wayahudi?”
34 [h]Yesu akamjibu, “Je, unauliza swali hili
kutokana na mawazo yako mwenyewe, au
uliambiwa na watu kunihusu mimi?”
35 [i]Pilato akamjibu, “Mimi si Myahudi,
ama sivyo? Taifa lako mwenyewe na
viongozi wa makuhani wamekukabidhi
kwangu. Umefanya kosa gani?”
36 [j]Yesu akajibu, “Ufalme wangu si wa
ulimwengu huu. Ufalme wangu ungekuwa
wa ulimwengu huu, wafuasi wangu
wangenipigania ili nisitiwe mikononi mwa
Wayahudi. Lakini kama ilivyo, ufalme
wangu hautoki hapa ulimwenguni.”
37 [k]Pilato akamuuliza, “Kwa hiyo wewe
ni mfalme?” Yesu akajibu, “Wewe wasema
kwamba mimi ni mfalme. Kwa kusudi hili
nilizaliwa, na kwa ajili ya hili nilikuja
ulimwenguni, ili niishuhudie kweli. Mtu
yeyote aliye wa kweli husikia sauti yangu.”
38 [l]Pilato akamuuliza Yesu, “Kweli ni
nini?” Baada ya kusema haya Pilato akaenda
nje tena akawaambia wale viongozi wa
Wayahudi waliomshtaki Yesu, “Sioni
kosa lolote alilotenda mtu huyu. 39 [m]Lakini
ninyi mna desturi yenu kwamba wakati wa
Pasaka nimwachie huru mfungwa mmoja
mnayemtaka. Je, mnataka niwafungulie
huyu ‘Mfalme wa Wayahudi’?”
40 [n]Wao wakapiga kelele wakisema, “Si
huyu mtu, bali tufungulie Baraba!” Yule
Baraba alikuwa mnyang’anyi.

*Yesu Ahukumiwa Kusulubiwa*

**(Mathayo 27:15-31; Marko 15:6-
20; Luka 23:13-25)**

19 [o]Ndipo Pilato akamtoa Yesu akaamuru
apigwe mijeledi. 2 Askari wakasokota

---

[a]**18:25** Yn 18:18; 18:17; Mt 26:69, 71; Mk 14:69; Lk 22:58
[b]**18:26** Yn 18:1; 10
[c]**18:27** Yn 13:38
[d]**18:28** Mt 27:2; Yn 18:33; 19:9; 11:55
[e]28 Jumba la mfalme la mtawala wa Kirumi lilikuwa linaitwa Praitorio.
[f]**18:32** Mt 20:19; 26:2
[g]**18:33** Mt 27:11; Yn 19:9; Lk 23:3; Mt 2:2
[h]**18:34** Mt 16:13
[i]**18:35** Yn 1:11; Mt 21:39
[j]**18:36** Mt 3:2; 26:53; Lk 17:21; Yn 6:51
[k]**18:37** Yn 3:32; 8:47; 1Yn 4:6
[l]**18:38** Lk 23:4-6
[m]**18:39** Mt 27:15; Mk 15:6; Lk 23:19
[n]**18:40** Mdo 3:14
[o]**19:1** Kum 25:3; Mt 27:26

taji ya miiba, wakamvika Yesu kichwani.
Wakamvalisha joho la zambarau.
3 [a]Wakawa wanapanda pale alipo tena
na tena, wakisema, “Salamu! Mfalme wa
Wayahudi!” Huku wakimpiga makofi usoni.
4 [b]Pilato akatoka tena nje akawaambia
wale waliokusanyika, “Tazameni,
namkabidhi Yesu kwenu kuwajulisha
kwamba mimi sikumwona ana hatia.”
5 [c]Kwa hiyo Yesu akatoka nje akiwa amevaa
ile taji ya miiba na lile vazi la zambarau.
Pilato akawaambia, “Tazameni, huyu hapa
huyo mtu!”
6 [d]Wale viongozi wa makuhani na maafisa
walipomwona, wakapiga kelele wakisema,
“Msulubishe! Msulubishe!”
Pilato akawaambia, “Mchukueni ninyi
mkamsulubishe, mimi sioni hatia juu yake.”
7 [e]Wayahudi wakamjibu, “Sisi tunayo
sheria na kutokana na sheria hiyo, hana
budi kufa kwa sababu yeye alijiita Mwana
wa Mungu.”
8 Pilato aliposikia haya, akaogopa
zaidi. 9 [f]Akaingia tena ndani ya jumba la
kifalme, akamuuliza Yesu, “Wewe umetoka
wapi?” Lakini Yesu hakumjibu. 10 Pilato
akamwambia, “Wewe unakataa kuongea
na mimi? Hujui ya kuwa nina mamlaka ya
kukuachia huru au kukusulubisha?”
11 [g]Ndipo Yesu akamwambia, “Wewe
hungekuwa na mamlaka yoyote juu yangu
kama hungepewa kutoka juu. Kwa hiyo
yeye aliyenitia mikononi mwako ana hatia
ya dhambi iliyo kubwa zaidi.”
12 [h]Tangu wakati huo, Pilato akajitahidi
kutafuta njia ya kumfungua Yesu, lakini
Wayahudi wakazidi kupiga kelele
wakisema, “Ukimwachia huyu mtu, wewe
si rafiki wa Kaisari. Mtu yeyote anayedai
kuwa mfalme anampinga Kaisari.”
13 [i]Pilato aliposikia maneno haya akamtoa
Yesu nje tena akaketi katika kiti chake cha
hukumu, mahali palipoitwa Sakafu ya Jiwe,
kwa Kiebrania paliitwa Gabatha[j] 14 [k]Basi
ilikuwa siku ya Maandalio ya Pasaka,
yapata kama saa sita hivi.
Pilato akawaambia Wayahudi, “Huyu
hapa mfalme wenu!”
15 [l]Wao wakapiga kelele, “Mwondoe!
Mwondoe! Msulubishe!”
Pilato akawauliza, “Je, nimsulubishe
mfalme wenu?”
Wale viongozi wa makuhani wakamjibu,
“Sisi hatuna mfalme mwingine ila Kaisari.”
16 [m]Ndipo Pilato akamkabidhi Yesu kwao
ili wamsulubishe.

*Kusulubiwa Kwa Yesu*

**(Mathayo 27:32-44; Marko 15:21-32; Luka 23:26-43)**

Kwa hiyo askari wakamchukua Yesu.
17 [n]Yesu, akiwa ameubeba msalaba wake,
akatoka kuelekea mahali palipoitwa Fuvu
la Kichwa (kwa Kiebrania ni Golgotha).
18 [o]Hapo ndipo walipomsulubisha. Pamoja
naye walisulubisha watu wengine wawili,
mmoja kila upande wake, naye Yesu
katikati.
19 [p]Pilato akaamuru tangazo liandikwe
na liwekwe juu kwenye msalaba wa Yesu,
likasema: “YESU WA NAZARETI, MFALME
WA WAYAHUDI.” 20 [q]Kwa kuwa mahali
hapo Yesu aliposulubiwa palikuwa karibu
na mjini, Wayahudi wengi walisoma
maandishi haya yaliyokuwa yameandikwa
kwa lugha za Kiebrania, Kiyunani na
Kilatini. 21 [r]Viongozi wa makuhani wa
Wayahudi wakapinga, wakamwambia
Pilato, “Usiandike ‘Mfalme wa Wayahudi,’

[a]**19:3** Mt 27:29; Yn 18:22
[b]**19:4** Yn 18:38; 19:6; Lk 23:4
[c]**19:5** Yn 19:2
[d]**19:6** Mdo 3:13; Yn 19:4; Lk 23:4
[e]**19:7** Law 24:16; Mt 26:63-66; Yn 5:18
[f]**19:9** Yn 18:33; Mk 14:61
[g]**19:11** Rum 13:1; Yn 18:28-30; Mdo 3:13
[h]**19:12** Lk 23:2
[i]**19:13** Mt 27:19; Yn 5:2
[j]13 Gabatha ni neno la Kiebrania ambalo maana yake ni Sakafu ya jiwe; ni mahali pa wazi palipoinuliwa ambako palitumika kama mahakama.
[k]**19:14** Mt 27:62; Mk 15:25
[l]**19:15** Yn 19:6
[m]**19:16** Mt 27:26; Mk 15:15
[n]**19:17** Mwa 22:6; Lk 14:27; 23:33; Yn 5:2
[o]**19:18** Lk 23:32
[p]**19:19** Mk 1:24; 14:21
[q]**19:20** Ebr 13:12
[r]**19:21** Yn 19:14

bali andika kwamba mtu huyu alisema yeye
ni mfalme wa Wayahudi.”
22 Pilato akawajibu, “Nilichokwisha
kuandika, nimeandika!”

*Mavazi Ya Yesu Yagawanywa*

23 [a]Askari walipokwisha kumsulubisha
Yesu, walichukua nguo zake wakazigawa
mafungu manne, kila askari fungu lake.
Ila walikubaliana wasilichane lile vazi
lake kwa maana lilikuwa halina mshono
bali limefumwa tangu juu hadi chini.
24 [b]Wakaambiana, “Tusilichane ila tulipigie
kura ili kuamua ni nani atalichukua.”
Hili lilitukia ili Maandiko yapate
kutimizwa yale yaliyosema,

> “Wanagawana nguo zangu,
> na vazi langu wanalipigia kura.”

Hayo ndiyo waliyoyafanya wale askari.
25 [c]Wakati huo huo karibu na msalaba
wa Yesu walikuwa wamesimama mama
yake, na dada wa mamaye, na Maria mke
wa Klopa, na Maria Magdalene. 26 [d]Yesu
alipomwona mama yake mahali pale
pamoja na yule mwanafunzi aliyempenda
wamesimama karibu, akamwambia mama
yake, “Mwanamke, huyo hapo ndiye
mwanao,” 27 [e]kisha akamwambia yule
mwanafunzi, “Nawe huyo hapo ndiye mama
yako.” Tangu wakati huo yule mwanafunzi
akamchukua mama yake Yesu nyumbani
kwake.

*Kifo Cha Yesu*

**(Mathayo 27:45-56; Marko 15:33-41; Luka 23:44-49)**

28 [f]Baada ya haya, Yesu hali akijua kuwa
mambo yote yamemalizika, alisema ili
kutimiza Maandiko, “Naona kiu.” 29 [g]Hapo
palikuwa na bakuli lililojaa siki. Kwa
hiyo wakachovya sifongo kwenye hiyo
siki, wakaiweka kwenye ufito wa mti wa
hisopo, wakampelekea mdomoni. 30 [h]Baada
ya kuionja hiyo siki, Yesu akasema,
“Imekwisha.” Akainamisha kichwa chake,
akaitoa roho yake.

*Yesu Achomwa Mkuki Ubavuni*

31 [i]Kwa kuwa ilikuwa siku ya Maandalio
ya Pasaka, Wayahudi hawakutaka miili
ibaki msalabani siku ya Sabato, hasa kwa
kuwa hiyo Sabato ingekuwa Sikukuu.
Wakamwomba Pilato aamuru miguu ya
wale waliosulubiwa ivunjwe ili wafe haraka
miili iondolewe kwenye misalaba. 32 [j]Kwa
hiyo askari wakaenda wakavunja miguu
ya mtu wa kwanza aliyesulubiwa pamoja
na Yesu na yule mwingine pia. 33 Lakini
walipomkaribia Yesu, wakaona ya kuwa
amekwisha kufa, hivyo hawakuvunja
miguu yake. 34 [k]Badala yake mmoja wa wale
askari akamchoma mkuki ubavuni na mara
pakatoka damu na maji. 35 [l]Mtu aliyeona
mambo hayo ndiye alitoa ushuhuda, nao
ushuhuda wake ni kweli. Anajua kuwa
anasema kweli, naye anashuhudia ili pia
nanyi mpate kuamini. 36 [m]Kwa maana
mambo haya yalitukia ili Maandiko yapate
kutimia, yale yasemayo, “Hakuna hata
mfupa wake mmoja utakaovunjwa.” 37 [n]Tena
Andiko lingine lasema, “Watamtazama yeye
waliyemchoma.”

*Maziko Ya Yesu*

**(Mathayo 27:57-61; Marko 15:42-47; Luka 23:50-56)**

38 Baada ya mambo haya, Yosefu wa
Arimathaya, aliyekuwa mfuasi wa Yesu,
ingawa kwa siri kwa sababu ya kuwaogopa
Wayahudi, alimwomba Pilato ruhusa
ili kuuchukua mwili wa Yesu. Pilato
alimruhusu, hivyo akaja, akauchukua.

---

[a]**19:23** Mt 27:35; Mk 15:24; Lk 23:34
[b]**19:24** Yn 19:28, 36, 37; Mt 1:22; Za 22:18
[c]**19:25** Mk 15:40, 41; Lk 23:49; Mt 12:46; Yn 13:23
[d]**19:26** Mt 12:46; Yn 13:23
[e]**19:27** Yn 1:11; 16:32
[f]**19:28** Za 69:21; Yn 19:30; 13:1; 19:24, 36, 37; Mt 1:22
[g]**19:29** Za 69:21; Mt 27:48
[h]**19:30** Lk 12:50
[i]**19:31** Yn 19:42; Mk 15:42; Kum 21:23
[j]**19:32** Yn 19:18
[k]**19:34** Zek 12:10; Ufu 1:7; 1Yn 5:6, 8
[l]**19:35** Lk 24:48; 15:27; 21:24
[m]**19:36** Yn 19:24, 28, 37; Mt 1:22; Kut 12:46; Hes 9:12; Za 34:20
[n]**19:37** Zek 12:10; Ufu 1:7

39 [a]Naye Nikodemo, yule ambaye kwanza alimwendea Yesu usiku, akaja, akaleta mchanganyiko wa manemane na manukato, yenye uzito wa zaidi ya kilo thelathini[b] 40 [c]Wakauchukua mwili wa Yesu, wakaufunga katika sanda ya kitani safi pamoja na yale manukato, kama ilivyokuwa desturi ya Wayahudi. 41 Basi palikuwa na bustani karibu na mahali pale aliposulubiwa, na pale ndani ya ile bustani palikuwa na kaburi jipya, ambalo halikuwa limezikiwa mtu bado. 42 Kwa hiyo, kwa kuwa ilikuwa siku ya Wayahudi ya Maandalio, nalo kaburi hilo lilikuwa karibu, wakamzika Yesu humo.

### *Kufufuka Kwa Yesu*

**(Mathayo 28:1-8; Marko 16:1-8; Luka 24:1-12)**

20 [d]Alfajiri na mapema siku ya kwanza ya juma, kulipokuwa kungali giza bado, Maria Magdalene alikwenda kaburini na kukuta lile jiwe limeondolewa penye ingilio. 2 [e]Hivyo akaja akikimbia kwa Simoni Petro pamoja na yule mwanafunzi mwingine ambaye Yesu alimpenda, na kusema, “Wamemwondoa Bwana kaburini, na hatujui walikomweka!”

3 [f]Petro na yule mwanafunzi mwingine wakaondoka mara kuelekea kaburini. 4 Wote wawili walikuwa wanakimbia, lakini yule mwanafunzi mwingine akakimbia mbio zaidi kuliko Petro, akatangulia kufika kaburini. 5 [g]Alipofika, akainama na kuchungulia mle kaburini, akaona vile vitambaa vya kitani mle ndani, lakini hakuingia. 6 Ndipo Simoni Petro akaja, akimfuata nyuma akaenda moja kwa moja hadi ndani ya kaburi. Naye akaona vile vitambaa vya ile sanda vikiwa pale chini 7 [h]na kile kitambaa kilichokuwa kichwani mwa Yesu. Kitambaa hicho kilikuwa kimekunjwa mahali pa peke yake, mbali na vile vitambaa vya kitani vya ile sanda. 8 [i]Kisha yule mwanafunzi aliyetangulia kufika kaburini naye akaingia ndani, akaona, akaamini, 9 [j](kwa kuwa mpaka wakati huo walikuwa bado hawajaelewa kutoka Maandiko kwamba ilikuwa lazima Yesu afufuke kutoka kwa wafu).

10 Kisha hao wanafunzi wakaondoka wakarudi nyumbani kwao.

### *Yesu Anamtokea Maria Magdalene*

**(Mathayo 28:9-10; Marko 16:9-11)**

11 [k]Lakini Maria Magdalene akasimama nje ya kaburi akilia. Alipokuwa akilia, akainama, kuchungulia mle kaburini, 12 [l]naye akaona malaika wawili wamevaa mavazi meupe, wameketi pale mwili wa Yesu ulipokuwa umelazwa, mmoja upande wa kichwani na mwingine upande wa miguuni.

13 [m]Wakamuuliza Maria, “Mwanamke, mbona unalia?”

Akawaambia, “Nalia kwa kuwa wamemchukua Bwana wangu na sijui walikomweka.” 14 [n]Baada ya kusema hayo, akageuka, akamwona Yesu amesimama, lakini hakumtambua.

15 [o]Yesu akamwambia, “Mwanamke, mbona unalia? Unamtafuta nani?”

Maria akidhani ya kuwa aliyekuwa anaongea naye ni mtunza bustani, kwa hiyo akamwambia, “Bwana, kama ni wewe umemchukua, tafadhali nionyeshe ulikomweka, nami nitamchukua.”

16 [p]Yesu akamwita, “Maria!”

Ndipo Maria akamgeukia Yesu na kusema naye kwa Kiebrania, “Rabboni!” (maana yake Mwalimu).

---

[a]**19:39** Yn 3:1; 7:50
[b]39 Zaidi ya kilo 30; tafsiri nyingine zinasema ratili 100, na nyingine ratili 75, ambazo ni kama kilo 34.
[c]**19:40** Ebr 13:12
[d]**20:1** Lk 8:2; Yn 19:25; Mt 27:60, 66
[e]**20:2** Yn 13:23
[f]**20:3** Lk 24:12
[g]**20:5** Yn 20:11; 19:40
[h]**20:7** Yn 11:44
[i]**20:8** Yn 20:4
[j]**20:9** Mt 22:29; Yn 2:22; Lk 24:26; Mdo 2:24
[k]**20:11** Yn 20:5
[l]**20:12** Mk 16:5; Mdo 10:30
[m]**20:13** Yn 20:2, 15
[n]**20:14** Mt 28:9; Mk 16:9; Lk 24:16; Yn 21:14
[o]**20:15** Yn 20:13
[p]**20:16** Yn 5:2; Mt 23:7

17 [a]Yesu akamwambia, “Usinishike, kwa
maana sijapaa kwenda kwa Baba. Lakini
nenda kwa ndugu zangu ukawaambie,
‘Ninapaa kwenda kwa Baba yangu ambaye
ni Baba yenu, kwa Mungu wangu ambaye
ni Mungu wenu.’ ”
18 [b]Kwa hiyo Maria Magdalene akaenda
kuwatangazia wanafunzi wa Yesu, akisema,
“Nimemwona Bwana!” Naye akawaambia
kwamba Yesu alikuwa amemweleza mambo
hayo yote.

### *Yesu Awatokea Wanafunzi Wake*

**(Mathayo 28:16-20; Marko 16:14-18; Luka 24:36-49)**

19 Ikawa jioni ya ile siku ya kwanza ya
juma, wanafunzi wake walikuwa pamoja,
milango ikiwa imefungwa kwa kuwaogopa
Wayahudi. Naye Yesu aliwatokea,
akasimama katikati yao, akasema, “Amani
iwe nanyi!”
20 [c]Baada ya kusema haya,
akawaonyesha mikono yake na ubavu
wake. Wanafunzi wake wakafurahi sana
walipomwona Bwana.
21 [d]Yesu akawaambia tena, “Amani iwe
nanyi! Kama vile Baba alivyonituma mimi,
mimi nami nawatuma ninyi.”
22 [e]Naye
alipokwisha kusema haya, akawavuvia,
akawaambia, “Pokeeni Roho Mtakatifu.
23 [f]Mkimwondolea mtu yeyote dhambi zake,
zitaondolewa, na yeyote msiyemwondolea
dhambi zake, hazitaondolewa.”

### *Yesu Anamtokea Tomaso*

24 [g]Lakini Tomaso, aliyeitwa Didimasi,
yaani Pacha, mmoja wa wale kumi na
wawili, hakuwa pamoja nao Yesu alipokuja.
25 [h]Hivyo wale wanafunzi wengine
wakamwambia, “Tumemwona Bwana.”
Lakini yeye akawaambia, “Nisipoona zile
alama za misumari mikononi mwake, na
kuweka kidole changu kwenye hizo alama
za misumari na mkono wangu ubavuni
mwake, sitaamini.”
26 [i]Baada ya siku nane, wanafunzi wake
walikuwa tena pamoja ndani ya nyumba,
naye Tomaso alikuwa pamoja nao. Ndipo
Yesu akaja milango ikiwa imefungwa na
kusimama katikati yao akasema, “Amani
iwe nanyi.”
27 [j]Kisha akamwambia Tomaso,
“Weka kidole chako hapa na uone mikono
yangu, nyoosha mkono wako uguse ubavuni
mwangu. Usiwe na shaka, bali uamini tu.”
28 [k]Tomaso akamwambia, “Bwana wangu
na Mungu wangu!”
29 [l]Yesu akamwambia, “Umeamini kwa
kuwa umeniona? Wamebarikiwa wale
ambao hawajaona lakini wameamini.”

### *Kusudi La Kitabu Hiki*

30 [m]Yesu alifanya miujiza mingine
mingi mbele za wanafunzi wake, ambayo
haikuandikwa katika kitabu hiki.
31 [n]Lakini
haya yameandikwa ili mweze kuamini
ya kuwa Yesu ndiye Kristo,[o] Mwana wa
Mungu, na kwa kumwamini mpate uzima
katika jina lake.

### *Yesu Awatokea Wanafunzi Saba*

21 [p]Baada ya haya Yesu akawatokea tena
wanafunzi wake kando ya Bahari ya
Tiberia.[q] Yeye alijionyesha kwao hivi:
2 [r]Simoni Petro, Tomaso aitwaye Didimasi,
yaani Pacha, Nathanaeli wa Kana ya
Galilaya, wana wa Zebedayo na wanafunzi
wengine wawili walikuwa pamoja.
3 [s]Simoni
Petro akawaambia wenzake, “Mimi naenda
kuvua samaki.” Nao wakamwambia,

---

[a]**20:17** Mt 28:10; Yn 7:33; Mt 28:10
[b]**20:18** Yn 20:1; Lk 24:10, 22, 23
[c]**20:20** Lk 24:36-39, 40; Yn 19:34; 16:20, 22; Lk 24:39, 40; Yn 19:34; 16:20
[d]**20:21** Yn 20:19; 3:17; Mt 28:19; Yn 17:18
[e]**20:22** Mdo 19:2; Gal 3:2; Yn 7:39; Mdo 2:38; 8:15; 17; 19:2; Gal 3:2
[f]**20:23** Mt 16:19; 18:18
[g]**20:24** Yn 11:16
[h]**20:25** Mk 16:11
[i]**20:26** Yn 14:27; 20:21
[j]**20:27** Yn 20:25; Lk 24:40
[k]**20:28** Yn 1:1; 20:29; 3:15; 1Pet 1:8
[l]**20:29** Yn 3:15; 1Pet 1:8
[m]**20:30** Yn 21:25; 2:11; 21:25; Mt 4; 3; 25:46
[n]**20:31** Yn 3:15; 19:35; Mt 4:3; 25:46
[o]31 *Kristo* maana yake ni *Masiya,* yaani *Aliyetiwa mafuta.*
[p]**21:1** Yn 21:14; 20:19, 26
[q]1 Yaani Bahari ya Galilaya.
[r]**21:2** Yn 11:16; 1:4; 2:1; Mt 4:21
[s]**21:3** Lk 5:5

“Tutakwenda pamoja nawe.” Wakatoka,
wakaingia ndani ya mashua, lakini usiku
ule hawakupata chochote.
4 [a]Mara baada ya kupambazuka, Yesu
akasimama ufuoni, lakini wanafunzi
hawakumtambua kwamba alikuwa Yesu.
5 [b]Yesu akawaambia, “Wanangu, je, mna
samaki wowote?”
Wakamjibu, “La.”
6 [c]Akawaambia, “Shusheni nyavu
upande wa kuume wa mashua yenu nanyi
mtapata samaki.” Wakashusha nyavu na
tazama wakapata samaki wengi mno hata
wakashindwa kuvutia zile nyavu zilizojaa
samaki ndani ya mashua.
7 [d]Yule mwanafunzi aliyependwa na Yesu
akamwambia Petro, “Huyu ni Bwana!”
Simoni Petro aliposikia haya, akajifunga
nguo yake kwa kuwa alikuwa uchi, naye
akajitosa baharini. 8 Wale wanafunzi
wengine wakaja kwa ile mashua huku
wakikokota ule wavu uliyojaa samaki,
maana hawakuwa mbali na nchi kavu,
ilikuwa yapata dhiraa 200[e] 9 [f]Walipofika
ufuoni, wakaona moto wa makaa na samaki
wakiokwa juu yake na mikate.
10 Yesu akawaambia, “Leteni baadhi ya
hao samaki mliovua sasa hivi.”
11 Simoni Petro akapanda kwenye mashua
na kuukokota ule wavu pwani. Ulikuwa
umejaa samaki wakubwa 153. Ingawa
samaki walikuwa wengi kiasi hicho, ule
wavu haukuchanika. 12 [g]Yesu akawaambia,
“Njooni mpate kifungua kinywa.” Hakuna
hata mmoja wa wanafunzi aliyethubutu
kumuuliza, “Wewe ni nani?” Kwa sababu
walijua ya kuwa ni Bwana. 13 [h]Yesu akaja,
akachukua ule mkate, akawapa na vivyo
hivyo akawagawia pia wale samaki. 14 [i]Hii
ilikuwa mara ya tatu Yesu kuwatokea
wanafunzi wake baada yake kufufuliwa
kutoka kwa wafu.

*Yesu Amuuliza Petro Kama Anampenda*

15 [j]Walipokwisha kula, Yesu akamuuliza
Simoni Petro, “Je, Simoni mwana wa
Yohana, unanipenda kweli kuliko hawa?”
Yeye akamjibu, “Ndiyo Bwana, wewe
unajua ya kuwa ninakupenda.”
Yesu akamwambia, “Lisha wana-kondoo
wangu.”
16 [k]Yesu akamwambia tena, “Simoni,
mwana wa Yohana, wanipenda?”
Petro akamjibu, “Ndiyo Bwana, wewe
unajua ya kuwa ninakupenda.”
Yesu akamwambia, “Chunga kondoo
zangu.”
17 [l]Kwa mara ya tatu Yesu akamuuliza
Petro, “Simoni mwana wa Yohana,
unanipenda?”
Petro akahuzunika sana kwa kuwa Yesu
alimuuliza mara ya tatu, “Unanipenda?”
Akamjibu, “Bwana, wewe unajua yote,
unajua ya kuwa ninakupenda.”
Yesu akamwambia, “Lisha kondoo wangu.
18 Amin, amin nakuambia, ulipokuwa
kijana ulivaa na kwenda unakotaka, lakini
utakapokuwa mzee utanyoosha mikono
yako na mtu mwingine atakuvika na
kukupeleka usipotaka kwenda.” 19 [m]Yesu
alisema haya ili kuashiria ni kifo cha aina
gani Petro atakachomtukuza nacho Mungu.
Kisha Yesu akamwambia Petro, “Nifuate!”
20 [n]Petro akageuka, akamwona yule
mwanafunzi aliyependwa na Yesu
akiwafuata. (Huyu ndiye yule mwanafunzi
aliyeegama kifuani mwa Yesu walipokula
naye chakula cha mwisho na kuuliza,
“Bwana, ni nani atakayekusaliti?”) 21 Petro
alipomwona huyo mwanafunzi, akamuuliza
Yesu, “Bwana na huyu je?”
22 [o]Yesu akamjibu, “Ikiwa nataka aishi
mpaka nitakaporudi, inakuhusu nini?

[a]**21:4** Lk 24:16; Yn 20:14
[b]**21:5** Lk 24:41
[c]**21:6** Lk 5:4-7
[d]**21:7** Yn 13:23
[e]8 Dhiraa 200 ni kama mita 90.
[f]**21:9** Yn 18:18; 21:10, 13
[g]**21:12** Mdo 10:41
[h]**21:13** Yn 21:9
[i]**21:14** Yn 20:19, 26
[j]**21:15** Lk 24:41
[k]**21:16** 2Sam 5:2; Mt 2:6
[l]**21:17** Yn 2:24, 25; 16:30
[m]**21:19** Yn 12:33; 18:32
[n]**21:20** Yn 16:22; 21:7; 13:23
[o]**21:22** Mt 16:27, 28; 25:31; 1Kor 4; 5; 11:26; Ufu 2:25; 3:11; 22:7, 20

Wewe inakupasa unifuate!”
23 [a]Kwa sababu ya maneno haya ya Yesu, uvumi ukaenea miongoni mwa ndugu kwamba huyu mwanafunzi hangekufa. Lakini Yesu hakusema kuwa hangekufa. Yeye alisema tu kwamba, “Ikiwa nataka aishi mpaka nitakaporudi, inakuhusu nini?”

24 [b]Huyu ndiye yule mwanafunzi anayeshuhudia mambo haya na ndiye ambaye ameandika habari hizi. Nasi tunajua ya kuwa ushuhuda wake ni kweli.

25 [c]Lakini kuna mambo mengine mengi ambayo Yesu alifanya. Kama yote yangeliandikwa, nadhani hata ulimwengu wote usingekuwa na nafasi ya kutosha kuweka vitabu vyote ambavyo vingeandikwa. Amen.

[a]**21:23** Mdo 1:16
[b]**21:24** Yn 15:27; 19:35
[c]**21:25** Yn 20:30

# MATENDO YA MITUME

*Mwandishi*

**KANISA LA KWANZA**

*(1:1–5:42)*

*Ahadi Ya Roho Mtakatifu*

1 [a]Katika kitabu changu cha kwanza
nilikuandikia, mpendwa Theofilo,
kuhusu mambo yote Yesu aliyofanya na
kufundisha tangu mwanzo, 2 [b]hadi siku ile
alipochukuliwa kwenda mbinguni, baada
ya kuwapa maagizo kupitia kwa Roho
Mtakatifu wale mitume aliowachagua.
3 [c]Baada ya mateso yake, alijionyesha kwao
na kuwathibitishia kwa njia nyingi kwamba
yeye yu hai. Katika muda wa siku arobaini
baada ya kufufuka kwake aliwatokea
na kunena kuhusu Ufalme wa Mungu.
4 [d]Wakati mmoja alipokuwa pamoja nao,
aliwapa amri hii, “Msitoke Yerusalemu, bali
ingojeni ahadi ya Baba, ambayo mmenisikia
nikisema habari zake. 5 [e]Yohana aliwabatiza
kwa maji, lakini baada ya siku chache
mtabatizwa kwa Roho Mtakatifu.”

*Yesu Apaa Mbinguni*

**(Marko 16:19-20; Luka 24:50-53)**

6 [f]Mitume walipokuwa wamekusanyika
pamoja, wakamuuliza Yesu, “Bwana, je,
huu ndio wakati wa kuwarudishia Israeli
ufalme?”

7 [g]Yesu akawaambia, “Si juu yenu kujua
nyakati na majira ambayo Baba ameyaweka
katika mamlaka yake mwenyewe. 8 [h]Lakini
mtapokea nguvu akiisha kuwajilia juu yenu
Roho Mtakatifu, nanyi mtakuwa mashahidi
wangu katika Yerusalemu, Uyahudi kote na
Samaria, hadi miisho ya dunia.”

9 [i]Baada ya kusema mambo haya,
walipokuwa wanatazama, akachukuliwa
juu mbinguni mbele ya macho yao na wingu
likampokea wasimwone tena.

10 [j]Walipokuwa bado wakikaza macho
yao kuelekea juu alipokuwa akienda zake
Mbinguni, tazama ghafula, wanaume wawili
waliovaa mavazi meupe wakasimama
karibu nao, 11 [k]wakasema, “Enyi watu wa
Galilaya, mbona mnasimama mkitazama
juu angani? Huyu Yesu aliyechukuliwa
kutoka kwenu kwenda Mbinguni, atarudi
tena jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda
zake Mbinguni.”

*Mathiya Achaguliwa Badala Ya Yuda*

**(Mathayo 27:3-10)**

12 [l]Ndipo waliporudi Yerusalemu kutoka
Mlima wa Mizeituni, uliokuwa karibu
na Yerusalemu, umbali wa mwendo wa
Sabato[m] kutoka mjini. 13 [n]Walipowasili
mjini Yerusalemu, walikwenda ghorofani
kwenye chumba walichokuwa wakiishi.
Wale waliokuwepo walikuwa: Petro,
Yohana, Yakobo, Andrea, Filipo, Tomaso,
Bartholomayo, Mathayo, Yakobo mwana wa
Alfayo, Simoni Zelote[o] na Yuda mwana wa
Yakobo. 14 [p]Hawa wote waliungana pamoja
katika maombi. Pamoja nao walikuwepo

---

[a]**1:1** Lk 1:14; 3:23
[b]**1:2** Mk 16:19; 6:30; Mt 28:19-20; 10:1-4; Yn 13:18
[c]**1:3** 1Kor 15:5-7; Mt 28:17; Lk 24:39-43
[d]**1:4** Lk 24:49; Yn 14:16; Mdo 2:33
[e]**1:5** Mk 1:4, 8; Mt 3:11; Mdo 11:16; 19:4; Yoe 3:18; Mdo 2:4; 11:15
[f]**1:6** Mt 17:11; Mdo 3:21; Lk 24:21; Isa 1:26; Dan 7:27; Amo 9:11
[g]**1:7** Za 102:13; Mt 24:48
[h]**1:8** Mdo 2:1-4; Lk 24:48
[i]**1:9** Mk 16:19; Lk 24:51; Yn 6:62
[j]**1:10** Lk 24:4; Yn 20:12; Mt 28:3; Mk 16:5; Mdo 10:3, 30
[k]**1:11** Mdo 2:7; Mt 16:27; Lk 21:27; 1Tim 3:16; Mdo 1:7
[l]**1:12** Lk 24:52; Mt 21:1
[m]12 Mwendo wa Sabato hapa ina maana umbali wa mita 1,100.
[n]**1:13** Mdo 9:37; 20:8; Mt 10:2-4; Mk 3:16-19
[o]13 Zelote hapa ina maana alikuwa mwanachama wa Wazelote, kikundi cha Kiyahudi cha kupinga jeuri ya Warumi.
[p]**1:14** Lk 18:1; 23:49-55; Mt 12:46

wanawake kadha, na Maria mama yake
Yesu, pamoja na ndugu zake Yesu.
15 [a]Katika siku hizo Petro akasimama
katikati ya waumini (jumla yao wote
walikuwa watu wapatao 120), akasema,
16 [b]“Ndugu zangu, ilibidi Andiko litimie
ambalo Roho Mtakatifu alitabiri kupitia
kwa Daudi kumhusu Yuda aliyewaongoza
wale waliomkamata Yesu. 17 [c]Yuda
alikuwa mmoja wetu, kwa maana na yeye
alichaguliwa ashiriki katika huduma hii.”
18 [d](Basi Yuda alinunua shamba kwa
zile fedha za uovu alizopata; akiwa huko
shambani akaanguka, akapasuka na
matumbo yote yakatoka nje. 19 [e]Kila mtu
Yerusalemu akasikia habari hizi, kwa hiyo
wakapaita mahali hapo kwa lugha yao,
Akeldama, yaani Shamba la Damu).
20 [f]“Kama vile ilivyoandikwa katika
kitabu cha Zaburi,

“ ‘Mahali pake na pawe ukiwa,
wala asiwepo yeyote atakayeishi
humo,’

na,

“ ‘Mtu mwingine aichukue nafasi
yake ya uongozi.’

21 [g]Kwa hiyo inatubidi tumchague mtu
mwingine miongoni mwa wale ambao
wamekuwa pamoja nasi wakati wote
Bwana Yesu alipoingia na kutoka katikati
yenu, 22 [h]kuanzia ubatizo wa Yohana mpaka
siku aliyochukuliwa kutoka kwetu kwenda
Mbinguni. Kwa kuwa mmoja wao inabidi
awe shahidi pamoja nasi wa ufufuo wake.”
23 [i]Wakapendekeza majina ya watu
wawili: Yosefu, aitwaye Barsaba (ambaye
pia alijulikana kama Yusto) na Mathiya.
24 [j]Kisha wakaomba, wakasema, “Bwana,
wewe waujua moyo wa kila mtu. Tuonyeshe
ni yupi kati ya hawa wawili uliyemchagua
25 [k]ili achukue nafasi ya huduma ya utume
ambayo Yuda aliiacha ili aende mahali pake
mwenyewe.” 26 [l]Kisha wakawapigia kura,
nayo kura ikamwangukia Mathiya, naye
akaongezwa kwenye wale mitume kumi
na mmoja.

*Kushuka Kwa Roho Mtakatifu*

2 [m]Siku ya Pentekoste ilipowadia, waamini
wote walikuwa mahali pamoja. 2 [n]Ghafula
sauti kama mvumo mkubwa wa upepo
mkali uliotoka mbinguni ukaijaza nyumba
yote walimokuwa wameketi. 3 [o]Zikatokea
ndimi kama za moto zilizogawanyika na
kukaa juu ya kila mmoja wao. 4 [p]Wote
wakajazwa na Roho Mtakatifu, wakaanza
kunena kwa lugha nyingine, kama Roho
alivyowajalia.
5 [q]Basi walikuwepo Yerusalemu Wayahudi
wanaomcha Mungu kutoka kila taifa chini
ya mbingu. 6 Waliposikia sauti hii, umati wa
watu ulikusanyika pamoja wakistaajabu,
kwa sababu kila mmoja wao aliwasikia
wakisema kwa lugha yake mwenyewe.
7 [r]Wakiwa wameshangaa na kustaajabu
wakauliza, “Je, hawa wote wanaozungumza
si Wagalilaya? 8 Imekuwaje basi kila mmoja
wetu anawasikia wakinena kwa lugha yake
ya kuzaliwa? 9 [s]Wapathi, Wamedi, Waelami,
wakazi wa Mesopotamia, Uyahudi,
Kapadokia, Ponto na Asia, 10 [t]Frigia,
Pamfilia, Misri na pande za Libya karibu na
Kirene na wageni kutoka Rumi, 11 Wayahudi
na waongofu, Wakrete na Waarabu, sote
tunawasikia watu hawa wakisema mambo
makuu ya ajabu ya Mungu katika lugha
zetu wenyewe.” 12 Wakiwa wameshangaa

[a]**1:15** Ufu 3:4
[b]**1:16** Mt 10:4; Yn 13:18
[c]**1:17** Yn 6:70-71; Mt 10:4; Lk 6:16; Mdo 12:25; 20:24; 21:19
[d]**1:18** Mt 26:14-15; 27:3-10
[e]**1:19** Yn 5:2
[f]**1:20** Za 69:25; 109:8
[g]**1:21** Yn 15:27
[h]**1:22** Mk 1:4; Lk 24:48
[i]**1:23** Mdo 15:22
[j]**1:24** Mdo 13:3; 14:23; 1Sam 16:7; Ufu 2:23
[k]**1:25** Mdo 1:17
[l]**1:26** Mdo 2:14
[m]**2:1** Law 23:15-16; 1Kor 16:18; Mdo 1:14
[n]**2:2** Mdo 4:31
[o]**2:3** Mt 3:11
[p]**2:4** Mk 16:17; 1Kor 12:10
[q]**2:5** Lk 2:25; Mdo 8:2
[r]**2:7** Mdo 1:11
[s]**2:9** Mdo 18:2; 1Pet 1:1; 2Kor 1:8; Ufu 1:4
[t]**2:10** Mdo 16:6; 18:23; 14:24; Mt 27:32

na kufadhaika wakaulizana, “Ni nini maana
ya mambo haya?”
13 [a]Lakini wengine wakawadhihaki
wakasema, “Hawa wamelewa divai!”

*Petro Ahutubia Umati*

14 Ndipo Petro akasimama pamoja na wale
mitume kumi na mmoja, akainua sauti yake
na kuhutubia ule umati wa watu, akasema:
“Wayahudi wenzangu na ninyi nyote mkaao
Yerusalemu, jueni jambo hili mkanisikilize.
15 [b]Hakika watu hawa hawakulewa kama
mnavyodhania, kwa kuwa sasa ni saa tatu
asubuhi! 16 [c]La, hili ni jambo lililotabiriwa
na nabii Yoeli, akisema:

17 [d]“ ‘Katika siku za mwisho, asema
Mungu,
nitamimina Roho wangu
juu ya wote wenye mwili.
Wana wenu na binti zenu watatabiri,
vijana wenu wataona maono,
na wazee wenu wataota ndoto.
18 [e]Hata juu ya watumishi wangu,
wanaume kwa wanawake,
katika siku zile nitamimina Roho
wangu,
nao watatabiri.
19 [f]Nami nitaonyesha maajabu juu
mbinguni,
na ishara chini duniani:
damu, moto, na mawimbi ya
moshi.
20 [g]Jua litakuwa giza
na mwezi utakuwa mwekundu
kama damu,
kabla ya kuja siku ile kuu ya Bwana
iliyo tukufu.
21 [h]Na kila mtu atakayeliitia
jina la Bwana, ataokolewa.’

22 [i]“Enyi Waisraeli, sikilizeni maneno
haya nisemayo: Yesu wa Nazareti alikuwa
mtu aliyethibitishwa kwenu na Mungu
kwa miujiza, maajabu na ishara, ambayo
Mungu alitenda miongoni mwenu kupitia
kwake, kama ninyi wenyewe mjuavyo.
23 [j]Huyu mtu akiisha kutolewa kwa shauri
la Mungu lililokusudiwa kwa kujua kwake
Mungu tangu zamani, ninyi, kwa mikono ya
watu wabaya, mlimuua kwa kumgongomea
msalabani. 24 [k]Lakini Mungu alimfufua
kutoka kwa wafu akamwondolea uchungu
wa mauti, kwa sababu haikuwezekana yeye
kushikiliwa na nguvu za mauti. 25 [l]Kwa
maana Daudi asema kumhusu yeye:

“ ‘Nalimwona Bwana mbele yangu
daima.
Kwa sababu yuko mkono wangu
wa kuume,
sitatikisika.
26 Kwa hiyo moyo wangu unafurahia,
na ulimi wangu unashangilia;
mwili wangu nao utapumzika kwa
tumaini.
27 [m]Kwa maana hutaniacha kaburini,
wala hutamwacha Aliye Mtakatifu
wako kuona uharibifu.
28 [n]Umenionyesha njia za uzima,
utanijaza na furaha mbele zako.’

29 [o]“Ndugu zangu Waisraeli, nataka
niwaambie kwa uhakika kwamba baba
yetu Daudi alikufa na kuzikwa, nalo
kaburi lake lipo hapa mpaka leo. 30 [p]Lakini
alikuwa nabii na alijua ya kuwa Mungu
alikuwa amemwahidi kwa kiapo kwamba
angemweka mmoja wa wazao wake penye
kiti chake cha enzi. 31 [q]Daudi, akiona mambo
yaliyoko mbele, akanena juu ya kufufuka
kwa Kristo,[r] kwamba hakuachwa kaburini,
wala mwili wake haukuona uharibifu.

[a]**2:13** 1Kor 14:23; Efe 5:18
[b]**2:15** 1The 5:7
[c]**2:16** Yoe 2:28-32
[d]**2:17** Eze 39:29; Yn 7:37-39; Mdo 21:9
[e]**2:18** Mdo 21:9-12; 1Kor 12:10, 28; 14:1
[f]**2:19** Yoe 2:30, 31; Lk 21:11
[g]**2:20** Mt 24:29
[h]**2:21** Yoe 2:28-32; Rum 10:13
[i]**2:22** Yn 4:48; Mdo 10:38; Yn 3:2
[j]**2:23** Isa 53:10; Lk 22:22; 24:20; Mt 16:21
[k]**2:24** Rum 8:11; Ebr 13:20; Yn 20:9
[l]**2:25** Za 16:8
[m]**2:27** Mdo 13:35
[n]**2:28** Za 16:8-11
[o]**2:29** Mdo 7:8-9; 1Fal 2:10; Neh 3:16
[p]**2:30** 2Sam 7:12; Mt 1:1; Za 132:11; Lk 1:32, 69; Rum 1:3; 2Tim 2:8
[q]**2:31** Za 16:10; Mdo 13:35
[r]31 *Kristo* maana yake ni *Masiya*, yaani *Aliyetiwa mafuta.*

32 [a]Mungu alimfufua huyu Yesu na sisi sote
ni mashahidi wa jambo hilo. 33 [b]Basi ikiwa
yeye ametukuzwa kwa mkono wa kuume
wa Mungu, amepokea kutoka kwa Baba
ahadi ya Roho Mtakatifu, naye amemimina
kile mnachoona sasa na kusikia. 34 [c]Kwa
kuwa Daudi hakupaa kwenda mbinguni,
lakini anasema,

" 'Bwana alimwambia Bwana
wangu:
"Keti mkono wangu wa kuume,
35 [d]hadi nitakapowaweka adui zako
chini ya miguu yako." '

36 [e]"Kwa hiyo Israeli wote na wajue
jambo hili kwa uhakika kwamba: Mungu
amemfanya huyu Yesu, ambaye ninyi
mlimsulubisha, kuwa Bwana na Kristo."

*Waumini Waongezeka*

37 [f]Watu waliposikia maneno haya
yakawachoma mioyo yao, wakawauliza
Petro na wale mitume wengine, "Ndugu
zetu tufanye nini?"
38 [g]Petro akawajibu, "Tubuni, mkabatizwe
kila mmoja wenu kwa jina la Yesu Kristo,
ili mpate kusamehewa dhambi zenu, nanyi
mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.
39 [h]Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu
na watoto wenu, na kwa wote walio mbali,
na kila mtu ambaye Bwana Mungu wetu
atamwita amjie."
40 [i]Petro akawaonya kwa maneno
mengine mengi na kuwasihi akisema,
"Jiepusheni na kizazi hiki kilichopotoka."
41 [j]Wale wote waliopokea ujumbe wa
Petro kwa furaha wakabatizwa na siku ile
waliongezeka watu wapatao 3,000.

*Ushirika Wa Waumini*

42 [k]Nao wakawa wanadumu katika
mafundisho ya mitume, katika ushirika,
katika kumega mkate na katika kusali.
43 [l]Kila mtu akaingiwa na hofu ya Mungu,
nayo miujiza mingi na ishara zikafanywa
na mitume. 44 [m]Walioamini wote walikuwa
mahali pamoja, nao walikuwa na kila
kitu shirika. 45 [n]Waliuza mali zao na vitu
walivyokuwa navyo, kila mtu akagawiwa
kadiri ya mahitaji yake. 46 [o]Siku zote kwa
moyo mmoja walikutana ndani ya ukumbi
wa Hekalu, wakimega mkate nyumba kwa
nyumba, wakila chakula chao kwa furaha
na moyo mweupe, 47 [p]wakimsifu Mungu
na kuwapendeza watu wote. Kila siku
Bwana akaliongeza kanisa wale waliokuwa
wakiokolewa.

*Petro Amponya Mlemavu Kwa Jina La Yesu*

3 [q]Siku moja Petro na Yohana walikuwa
wanapanda kwenda Hekaluni kusali
yapata saa tisa alasiri. 2 [r]Basi palikuwa
na mtu mmoja aliyekuwa kiwete tangu
kuzaliwa. Alichukuliwa na kuwekwa
kwenye lango la Hekalu liitwalo Zuri,
kila siku ili aombe msaada kwa watu
wanaoingia Hekaluni. 3 Huyu mtu
alipowaona Petro na Yohana wakikaribia
kuingia Hekaluni, akawaomba wampe
sadaka. 4 [s]Wakamkazia macho, kisha Petro
akamwambia, "Tutazame sisi." 5 Hivyo yule
mtu akawatazama, akitazamia kupata kitu
kutoka kwao.
6 [t]Ndipo Petro akamwambia, "Sina
fedha wala dhahabu, lakini nilicho nacho
ndicho nikupacho. Kwa jina la Yesu
Kristo wa Nazareti, tembea!" 7 Petro
akamshika yule mtu kwa mkono wa
kuume akamwinua, mara nyayo zake na

[a]**2:32** Mdo 1:8; 2:24; Lk 24:48
[b]**2:33** Flp 2:9; Mk 16:19; Yn 14:26; Mdo 10:45; Yn 15:26
[c]**2:34** Za 110:1; Mt 22:44; 1Kor 15:25; Efe 1:20; Ebr 1:13
[d]**2:35** Za 110:1; Mt 22:44
[e]**2:36** Lk 2:11; Mdo 5:31; Mt 28:18
[f]**2:37** Lk 3:10-14; Mdo 16:30
[g]**2:38** Mdo 22:16; Kol 2:12; Yer 36:3
[h]**2:39** Isa 44:3; 66:23; 57:19; Efe 2:13
[i]**2:40** Kum 32:5; Flp 2:15
[j]**2:41** Mdo 2:47; 4:4; 5:14; 9:31, 35, 42; 11:21, 24; 14:1, 21
[k]**2:42** Mdo 1:14
[l]**2:43** Mdo 5:12
[m]**2:44** Mdo 4:32
[n]**2:45** Mt 19:21; Lk 12:33
[o]**2:46** Lk 24:53; Mdo 3:1; 20:7; Mt 14:19
[p]**2:47** Rum 14:18; Mdo 5:14
[q]**3:1** Lk 22:8; Mdo 2:46; Za 55:17; Mdo 10:30
[r]**3:2** Mdo 14:8; Lk 16:20; Yn 9:8
[s]**3:4** Mdo 14:9
[t]**3:6** Mk 1:24; Mdo 14:10

vifundo vya miguu yake vikapata nguvu.
8 [a]Akaruka juu na kusimama, akaanza
kutembea. Kisha akaingia Hekaluni pamoja
na Petro na Yohana, huku akitembea na
kurukaruka na kumsifu Mungu. 9 [b]Watu
wote walipomwona akitembea na kumsifu
Mungu, 10 [c]wakamtambua kuwa ni yule mtu
aliyekuwa akiketi nje ya Hekalu penye
lango liitwalo Zuri akiomba msaada, nao
wakajawa na mshangao, wakastaajabu juu
ya yale yaliyomtukia.

### *Petro Anashuhudia Kuwa Yesu Anaponya*

11 [d]Aliyeponywa alipokuwa akiambatana
na Petro na Yohana, watu wote walishangaa
mno, wakaja wakiwakimbilia pale ukumbi
wa Solomoni. 12 Petro alipoona watu
wamekusanyika akawaambia, “Enyi
Waisraeli, kwa nini mnastaajabu kuhusu
jambo hili? Mbona mnatukazia macho kwa
mshangao kana kwamba ni kwa uwezo
wetu au utakatifu wetu tumemfanya mtu
huyu kutembea? 13 [e]Mungu wa Abrahamu
na Isaki na Yakobo, Mungu wa baba zetu
amemtukuza Mwanawe Yesu, ambaye ninyi
mlimtoa ahukumiwe kifo na mkamkana
mbele ya Pilato, ingawa yeye alikuwa
ameamua kumwachia aende zake. 14 [f]Ninyi
mlimkataa huyo Mtakatifu na Mwenye Haki
mkaomba mpewe yule muuaji. 15 [g]Hivyo
mkamuua aliye chanzo cha uzima, lakini
Mungu akamfufua kutoka kwa wafu. Sisi tu
mashahidi wa mambo haya. 16 [h]Kwa imani
katika jina la Yesu, huyu mtu mnayemwona
na kumfahamu ametiwa nguvu. Ni kwa jina
la Yesu na imani itokayo kwake ambayo
imemponya kabisa huyu mtu, kama ninyi
wote mnavyoona.
17 [i]“Sasa ndugu zangu, najua ya kuwa ninyi
mlitenda bila kujua, kama walivyofanya
viongozi wenu. 18 [j]Lakini kwa njia hii Mungu
alitimiza kile ambacho alikuwa ametabiri
kwa vinywa vya manabii wake wote,
kwamba Kristo[k] atateswa. 19 [l]Tubuni basi
mkamgeukie Mungu, dhambi zenu zifutwe,
ili zipate kuja nyakati za kuburudishwa
kwa kuwepo kwake Bwana, 20 [m]naye apate
kumtuma Kristo, ambaye ameteuliwa kwa
ajili yenu, yaani Yesu. 21 [n]Ilimpasa mbingu
zimpokee mpaka wakati wa kufanywa
upya kila kitu, kama Mungu alivyoahidi
zamani kupitia kwa vinywa vya manabii
wake watakatifu. 22 [o]Kwa maana Mose
alisema, ‘Bwana Mungu wenu atawainulia
nabii kama mimi kutoka miongoni mwa
ndugu zenu. Itawapasa kumtii huyo
kwa kila jambo atakalowaambia. 23 [p]Mtu
yeyote ambaye hatamsikiliza huyo nabii,
atatupiliwa mbali kabisa na watu wake.’
24 [q]“Naam, manabii wote tangu Samweli
na waliokuja baada yake, wote walitabiri
kuhusu siku hizi. 25 [r]Ninyi ndio wana wa
manabii na wa Agano ambalo Mungu
alifanya na baba zenu, akimwambia
Abrahamu, ‘Kupitia kwa uzao wako,
watu wote wa ulimwengu watabarikiwa.’
26 [s]Mungu alipomfufua Yesu Mwanawe,
alimtuma kwenu kwanza, ili awabariki kwa
kumgeuza kila mmoja wenu kutoka njia
yake mbaya.”

### *Petro Na Yohana Mbele Ya Baraza*

4 [t]Wakati Petro na Yohana walipokuwa
wakisema na watu, makuhani, mkuu
wa walinzi wa Hekalu na Masadukayo
wakawajia, 2 [u]huku wakiwa wamekasirika
sana kwa sababu mitume walikuwa

[a]**3:8** Isa 35:6; Mdo 14:10
[b]**3:9** Mdo 4:16, 21
[c]**3:10** Mdo 3:2; Yn 9:8
[d]**3:11** Lk 22:8; Yn 10:23; Mdo 5:12
[e]**3:13** Mdo 7:32; 22:14; Mt 27; 2; Lk 23:4
[f]**3:14** Mdo 4:27; 7:52; Mk 15:11; Lk 23:18-25
[g]**3:15** Mdo 2:24; 2:32
[h]**3:16** Mt 9:22; Mdo 4:10; 14:9
[i]**3:17** Lk 23:34; Mdo 13:27
[j]**3:18** Mdo 17:2-3; Lk 24:27; Mdo 26:22-27
[k]18 *Kristo* maana yake ni *Masiya*, yaani *Aliyetiwa mafuta.*
[l]**3:19** Za 5:11; Mdo 2:38
[m]**3:20** Lk 2:11
[n]**3:21** Mdo 1:11; Mt 17:11; Lk 1:70
[o]**3:22** Kum 18:15-18; Mdo 7:37
[p]**3:23** Kum 18:19; Law 23:29
[q]**3:24** Lk 24:27
[r]**3:25** Mdo 2:39; Rum 9:4-5; Mwa 22:18; 28:14
[s]**3:26** Mdo 2:24; 13:46; Rum 1:16
[t]**4:1** Lk 22:4; Mt 3:7; 16:1-6
[u]**4:2** Mdo 17:18

wanawafundisha watu na kuhubiri
kwamba kuna ufufuo wa wafu ndani ya
Yesu. 3 [a]Wakawakamata Petro na Yohana
na kuwatia gerezani mpaka kesho yake
kwa kuwa ilikuwa jioni. 4 [b]Lakini wengi
waliosikia lile neno waliamini, idadi yao
ilikuwa yapata wanaume 5,000.

5 [c]Kesho yake, viongozi wa Kiyahudi,
wazee na walimu wa sheria wakakusanyika
Yerusalemu. 6 [d]Walikuwepo kuhani mkuu
Anasi, Kayafa, Yohana, Iskanda, na wengi
wa jamaa ya kuhani mkuu. 7 [e]Baada ya
kuwasimamisha Petro na Yohana katikati
yao, wakawauliza, "Ni kwa uwezo gani au
kwa jina la nani mmefanya jambo hili?"

8 [f]Petro, akiwa amejaa Roho Mtakatifu,
akajibu, "Enyi watawala na wazee wa
watu, 9 [g]kama leo tukihojiwa kwa habari ya
mambo mema aliyotendewa yule kiwete na
kuulizwa jinsi alivyoponywa, 10 [h]ijulikane
kwenu nyote na kwa watu wote wa Israeli
kwamba: Ni kwa jina la Yesu Kristo wa
Nazareti, ambaye ninyi mlimsulubisha
lakini Mungu akamfufua kutoka kwa wafu,
kwa jina hilo mtu huyu anasimama mbele
yenu akiwa mzima kabisa. 11 [i]Huyu ndiye

" 'jiwe ambalo ninyi wajenzi
mlilikataa,
ambalo limekuwa jiwe kuu la
pembeni.'

12 [j]Wala hakuna wokovu katika mwingine
awaye yote, kwa maana hakuna jina jingine
chini ya mbingu walilopewa wanadamu
litupasalo sisi kuokolewa kwalo."

*Ujasiri Wa Petro Na Yohana Washangaza Watu*

13 [k]Wale viongozi na wazee walipoona
ujasiri wa Petro na Yohana na kujua ya
kuwa walikuwa watu wa kawaida, wasio
na elimu, walishangaa sana, wakatambua
kwamba hawa watu walikuwa na Yesu.
14 [l]Lakini kwa kuwa walikuwa wanamwona
yule kiwete aliyeponywa amesimama pale
pamoja nao, hawakuweza kusema lolote
kuwapinga. 15 [m]Wakawaamuru watoke
nje ya Baraza la Wayahudi[n] wakati
wakisemezana jambo hilo wao kwa wao.
16 [o]Wakaulizana, "Tuwafanyie nini watu
hawa? Hatuwezi kukanusha muujiza huu
mkubwa walioufanya ambao ni dhahiri kwa
kila mtu Yerusalemu. 17 [p]Lakini ili kuzuia
jambo hili lisiendelee kuenea zaidi kwa
watu, ni lazima tuwaonye watu hawa ili
wasiseme tena na mtu yeyote kwa jina la
Yesu." 18 [q]Kisha wakawaita tena ndani na
kuwaamuru wasiseme wala kufundisha
kamwe kwa hili jina la Yesu.

*Imetupasa Kumtii Mungu Kuliko Wanadamu*

19 [r]Lakini Petro na Yohana wakajibu,
"Amueni ninyi wenyewe iwapo ni haki
mbele za Mungu kuwatii ninyi kuliko kumtii
Mungu. 20 [s]Lakini sisi hatuwezi kuacha
kusema yale tuliyoyaona na kuyasikia."

21 [t]Baada ya vitisho vingi, wakawaacha
waende zao. Hawakuona njia yoyote ya
kuwaadhibu, kwa sababu ya watu, kwa
kuwa watu wote walikuwa wakimsifu
Mungu kwa kile kilichokuwa kimetukia.
22 Kwa kuwa umri wa yule mtu aliyekuwa
ameponywa kwa muujiza ulikuwa zaidi ya
miaka arobaini.

*Maombi Ya Waumini*

23 [u]Punde Petro na Yohana walipoachiliwa,
walirudi kwa waumini wenzao wakawaeleza

[a]**4:3** Mdo 5:18
[b]**4:4** Mdo 2:41
[c]**4:5** Lk 23:13
[d]**4:6** Mt 26:3; Lk 3:2
[e]**4:7** Kut 2:14; Mt 21:23; Mdo 7:27
[f]**4:8** Lk 23:13; Mt 10:19, 20
[g]**4:9** Mdo 3:6
[h]**4:10** Mdo 2:24; Mk 1:24
[i]**4:11** Zek 10:4; Efe 2:20
[j]**4:12** Yn 14:6; Rum 11:14
[k]**4:13** Lk 22:8; Mt 11:25
[l]**4:14** Mdo 3:8, 9; 3:11
[m]**4:15** Mt 5:22
[n]15 *Baraza la Wayahudi* hapa ina maana ya *Sanhedrin* ambalo lilikuwa ndilo baraza la juu kabisa la utawala wa Kiyahudi, lililoundwa na wazee 70 pamoja na kuhani mkuu.
[o]**4:16** Yn 11:47; Mdo 3:6-10
[p]**4:17** Mdo 5:28
[q]**4:18** Amo 7:13; Mdo 5:40
[r]**4:19** Mdo 5:29
[s]**4:20** Mdo 1:8; 2:32; 22; 15; 1Yn 1:1, 3
[t]**4:21** Mdo 5:26; Mt 9:8
[u]**4:23** Mdo 12; 12

waliyoambiwa na viongozi wa makuhani
na wazee. 24 [a]Watu waliposikia hayo,
wakainua sauti zao, wakamwomba Mungu kwa pamoja, wakisema, "Bwana Mwenyezi, uliyeziumba mbingu na nchi na bahari, na
vitu vyote vilivyomo. 25 [b]Wewe ulisema kwa
Roho Mtakatifu kupitia kwa kinywa cha baba yetu Daudi, mtumishi wako, ukasema:

" 'Mbona mataifa wanaghadhibika,
na kabila za watu zinawaza
ubatili?
26 [c]Wafalme wa dunia wamejipanga,
na watawala wanakusanyika
pamoja
dhidi ya Bwana
na dhidi ya Mpakwa Mafuta
wake.'

27 [d]Ni kweli Herode na Pontio Pilato pamoja na watu wa Mataifa na Waisraeli, walikusanyika katika mji huu dhidi ya mwanao mtakatifu Yesu uliyemtia mafuta.
28 [e]Wao wakafanya yale ambayo uweza wako na mapenzi yako yalikuwa yamekusudia
yatokee tangu zamani. 29 [f]Sasa, Bwana angalia vitisho vyao na utuwezeshe sisi watumishi wako kulinena neno lako kwa
ujasiri mkuu. 30 [g]Nyoosha mkono wako ili kuponya wagonjwa na kutenda ishara na miujiza kwa jina la Mwanao mtakatifu Yesu."
31 [h]Walipokwisha kuomba, mahali walipokuwa wamekutanika pakatikiswa, wote wakajazwa na Roho Mtakatifu, wakanena neno la Mungu kwa ujasiri.

*Walioamini Washirikiana Mali Zao*

32 [i]Wale walioamini wote walikuwa na moyo mmoja na nia moja. Wala hakuna hata mmoja aliyesema chochote alichokuwa
nacho ni mali yake mwenyewe, lakini walishirikiana kila kitu walichokuwa nacho.
33 [j]Mitume wakatoa ushuhuda wa kufufuka kwa Bwana Yesu kwa nguvu nyingi na neema ya Mungu ilikuwa juu yao wote.
34 [k]Wala hapakuwepo mtu yeyote miongoni mwao aliyekuwa mhitaji, kwa sababu mara kwa mara wale waliokuwa na mashamba na nyumba waliviuza, wakaleta thamani ya
vitu vilivyouzwa, 35 [l]wakaiweka miguuni pa mitume, kila mtu akagawiwa kadiri ya mahitaji yake.
36 [m]Yosefu, Mlawi kutoka Kipro, ambaye mitume walimwita Barnaba (maana yake
Mwana wa Faraja), 37 [n]aliuza shamba alilokuwa nalo, akaleta hizo fedha alizopata na kuziweka miguuni pa mitume.

*Anania Na Safira*

5 Lakini mtu mmoja jina lake Anania pamoja na mkewe Safira waliuza
kiwanja. 2 [o]Huku mkewe akijua kikamilifu,
Anania alificha sehemu ya fedha alizopata, akaleta kiasi kilichobaki na kukiweka miguuni pa mitume.
3 [p]Petro akamuuliza, "Anania, mbona Shetani ameujaza moyo wako ili kumwambia uongo Roho Mtakatifu, ukaficha sehemu ya
fedha ulizopata kutokana na kiwanja? 4 [q]Je,
kabla hujauza hicho kiwanja si kilikuwa mali yako? Hata baada ya kukiuza, fedha ulizopata si zilikuwa kwenye uwezo wako? Kwa nini basi umewaza hila hii moyoni mwako kufanya jambo kama hili? Wewe hukumwambia uongo mwanadamu bali Mungu."
5 [r]Anania aliposikia maneno haya akaanguka chini na kufa. Hofu kuu ikawapata wote waliosikia jambo lililokuwa
limetukia. 6 [s]Vijana wakaja, wakaufunga

[a]**4:24** 2Fal 19:15; Kut 20:11; Za 146:6; Isa 37:16; Lk 2:29; Ufu 6:10
[b]**4:25** Za 2:1, 2
[c]**4:26** Dan 9:25; Lk 4:18
[d]**4:27** Mt 14:1; 27:2; Lk 23:12; Mdo 3:13-14
[e]**4:28** Mdo 2:23
[f]**4:29** Za 138:3; Efe 6:19
[g]**4:30** Yn 4:48
[h]**4:31** Mdo 2:2, 4; 16:26; Lk 1:15; Ebr 4:12
[i]**4:32** Mdo 2:44
[j]**4:33** Lk 24:48; Mdo 1:22
[k]**4:34** Mt 19; 21; Mdo 2:45
[l]**4:35** Mdo 5:2; 2:45; 6:1
[m]**4:36** 1Kor 9:6; Gal 2:1, 9-13
[n]**4:37** Mdo 5:2
[o]**5:2** Mdo 4:35-37
[p]**5:3** Mt 4:10; Yn 13:2, 27
[q]**5:4** Kum 23:22; Law 6:2
[r]**5:5** Za 5:6; Mdo 5:10
[s]**5:6** Yn 19:40

mwili wake sanda, wakamchukua nje
kumzika.
7 Saa tatu baadaye mkewe Anania
akaingia, naye hana habari ya mambo
yaliyotukia. 8 [a]Petro akamuuliza, "Niambie,
je, mliuza kiwanja kwa thamani hii?"
Akajibu, "Ndiyo, tuliuza kwa thamani
hiyo."
9 [b]Ndipo Petro akamwambia, "Imekuwaje
mkakubaliana kumjaribu Roho wa Bwana?
Tazama! Nyayo za vijana waliomzika
mumeo ziko mlangoni, wewe nawe
watakuchukua nje."
10 [c]Saa ile ile akaanguka chini miguuni
mwake na kufa. Nao wale vijana wakaingia,
wakamkuta amekufa, wakamchukua
wakamzika kando ya mumewe. 11 [d]Hofu kuu
ikalipata kanisa lote pamoja na watu wote
waliosikia juu ya matukio haya.

### *Mitume Waponya Wengi*

12 [e]Mitume wakafanya ishara nyingi na
miujiza miongoni mwa watu. Walioamini
wote walikuwa wakikusanyika katika
ukumbi wa Solomoni. 13 [f]Hakuna mtu
mwingine aliyethubutu kuambatana nao
ijapokuwa waliheshimiwa sana na watu.
14 [g]Hata hivyo, waliomwamini Bwana
wakazidi kuongezeka, wanaume na
wanawake. 15 [h]Hata wakawa wanawaleta
wagonjwa na kuwalaza kwenye magodoro
na kwenye vitanda barabarani ili yamkini
Petro akipita kivuli chake kiwaguse baadhi
yao. 16 [i]Pia watu wakakusanyika kutoka
miji iliyokuwa karibu na Yerusalemu,
wakileta wagonjwa na watu walioteswa
na pepo wachafu. Hao wote wakaponywa.

### *Mitume Washtakiwa*

17 [j]Kisha kuhani mkuu na wenzake wote
waliokuwa pamoja naye, waliokuwa wa
kundi la Masadukayo, wakajawa na wivu.
18 Wakawakamata mitume na kuwatia
gerezani. 19 [k]Lakini wakati wa usiku,
malaika wa Bwana akaja, akafungua
milango ya gereza na akawatoa nje.
Akawaambia, 20 [l]"Nendeni, mkasimame
Hekaluni mkawaambie watu maneno yote
ya uzima huu mpya."
21 [m]Waliposikia haya wakaenda Hekaluni
alfajiri wakaendelea kufundisha watu.

Kuhani mkuu na wale waliokuwa pamoja
nao walipowasili, alikusanya baraza na
wazee wote wa Israeli wakatuma wale
mitume waletwe kutoka gerezani. 22 [n]Lakini
wale walinzi wa Hekalu walipokwenda
gerezani hawakuwakuta mitume mle.
Kwa hiyo wakarudi na kutoa habari.
23 Wakasema, "Tumekuta milango ya
gereza imefungwa sawasawa na askari wa
gereza wamesimama nje ya mlango, lakini
tulipofungua milango hakuwepo mtu yeyote
ndani." 24 [o]Basi mkuu wa walinzi wa Hekalu
na viongozi wa makuhani waliposikia haya,
wakafadhaika na kushangaa sana kwa ajili
yao kwamba jambo hili litakuwaje.
25 Ndipo mtu mmoja akaja akawaambia,
"Tazameni watu mliowatia gerezani wako
Hekaluni wakiwafundisha watu." 26 [p]Ndipo
yule mkuu wa walinzi wa Hekalu wakaenda
pamoja na askari wakawaleta wale mitume,
lakini bila ghasia kwa sababu waliogopa
kupigwa mawe na watu.
27 [q]Wakiisha kuwaleta mitume
wakawaamuru kusimama mbele ya baraza
ili kuhani mkuu awahoji. 28 [r]"Tuliwaonya
kwa nguvu msifundishe kwa jina hili,
lakini ninyi mmeijaza Yerusalemu yote
mafundisho yenu na tena mmekusudia
kuleta damu ya mtu huyu juu yetu."
29 [s]Petro na wale mitume wengine

---

[a]**5:8** Mdo 5:2
[b]**5:9** Mdo 5:3; Mt 4:7
[c]**5:10** Mdo 5:5, 6
[d]**5:11** Mdo 19:7
[e]**5:12** Yn 4:48; Mdo 2:43; 4:32; Yn 10:23
[f]**5:13** Mdo 2:47; 4:21; Yn 9:22; 12:42; 19; 18
[g]**5:14** Mdo 2:41, 47; 6; 7; 21:20
[h]**5:15** Mdo 19; 12
[i]**5:16** Mt 8:16; Mk 16:17
[j]**5:17** Mdo 15:5; 4:1
[k]**5:19** Kut 3:2; Mt 28:2; Mdo 16:26
[l]**5:20** Yn 6:63-68; 17:3; 1Yn 5:11
[m]**5:21** Mdo 4:5-6; Mt 5:22
[n]**5:22** Mdo 12:18, 19
[o]**5:24** Lk 22:4; Mdo 4:1
[p]**5:26** Mdo 4:21
[q]**5:27** Mt 5:22
[r]**5:28** Mdo 4:18; Mt 23:35; 27:25
[s]**5:29** Kut 1:17; Mdo 4:19

wakajibu, “Imetupasa kumtii Mungu
kuliko wanadamu. 30 [a]Mungu wa baba
zetu alimfufua Yesu kutoka kwa wafu,
ambaye ninyi mlimuua kwa kumtundika
kwenye msalaba. 31 [b]Mungu alimtukuza,
akamweka mkono wake wa kuume kuwa
Kiongozi na Mwokozi ili awape Israeli
toba na msamaha wa dhambi. 32 [c]Nasi tu
mashahidi wa mambo haya, vivyo hivyo na
Roho Mtakatifu ambaye Mungu amewapa
wale wanaomtii.”

33 [d]Wale wajumbe wa baraza la wazee
waliposikia haya, walijawa na ghadhabu,
wakataka kuwaua mitume. 34 [e]Lakini Farisayo
mmoja, jina lake Gamalieli, aliyekuwa
mwalimu wa sheria, aliyeheshimiwa na
watu wote, akasimama mbele ya baraza
akaamuru mitume watolewe nje kwa muda.
35 Ndipo alipowaambia wajumbe wa baraza,
“Enyi watu wa Israeli, fikirini kwa uangalifu
mnayotaka kuwatendea watu hawa. 36 [f]Kwa
maana wakati uliopita, aliinuka mtu mmoja
jina lake Theuda, alijidai kuwa yeye ni
mtu maarufu, akapata wafuasi wapatao
400 walioambatana naye. Lakini aliuawa,
na wafuasi wake wote wakatawanyika,
wakawa si kitu. 37 [g]Baada yake, alitokea
Yuda Mgalilaya wakati wa kuorodhesha
watu, naye akaongoza kundi la watu
kuasi. Yeye pia aliuawa, nao wafuasi wake
wakatawanyika. 38 [h]Kwa hiyo, kwa habari
ya jambo hili nawashauri, jiepusheni na
watu hawa. Waacheni waende zao! Kwa
maana kama kusudi lao na shughuli yao
imetokana na mwanadamu, haitafanikiwa.
39 [i]Lakini ikiwa imetoka kwa Mungu,
hamtaweza kuwazuia watu hawa. Badala
yake mtajikuta mnapigana na Mungu.”

40 [j]Wakapokea ushauri wa Gamalieli.
Wakawaita mitume ndani, wakaamuru
wachapwe mijeledi, kisha wakawaagiza
wasinene tena kwa jina la Yesu,
wakawaachia waende zao.

41 [k]Nao mitume wakatoka nje ya baraza,
wakiwa wamejaa furaha kwa sababu
wamehesabiwa kustahili kupata aibu kwa
ajili ya jina la Yesu. 42 [l]Kila siku, Hekaluni
na nyumba kwa nyumba, hawakuacha
kufundisha na kuhubiri habari njema
kwamba Yesu ndiye Kristo.[m]

## MATESO NA KUENEA KWA INJILI

*(6:1–9:31)*

*Saba Wachaguliwa Kuhudumu*

1 [n]Basi ikawa katika siku hizo, wakati
idadi ya wanafunzi ilipokuwa ikiongezeka
sana, palitokea manung’uniko kati ya
Wayahudi wa Kiyunani, dhidi ya Waebrania
kwa sababu wajane wao walisahaulika
katika mgawanyo wa chakula wa kila
siku. 2 [o]Wale mitume kumi na wawili
wakakusanya wanafunzi wote pamoja
wakasema, “Haitakuwa vyema sisi kuacha
huduma ya neno la Mungu ili kuhudumu
mezani. 3 [p]Kwa hiyo ndugu, chagueni watu
saba miongoni mwenu, watu wenye sifa
njema, waliojawa na Roho Mtakatifu na
hekima, ambao tunaweza kuwakabidhi kazi
hii, 4 [q]nasi tutatumia muda wetu kuomba na
huduma ya neno.”

5 [r]Yale waliyosema yakawapendeza watu
wote, nao wakamchagua Stefano (mtu
aliyejawa na imani na Roho Mtakatifu)
pamoja na Filipo, Prokoro, Nikanori,
Timoni, Parmena na Nikolao, mwongofu
kutoka Antiokia. 6 [s]Wakawaleta watu hawa
mbele ya mitume, nao wakawaombea na
kuwawekea mikono juu yao.

---

[a]**5:30** Mdo 3:13; 2:24; Gal 3:13; 1Pet 2:24
[b]**5:31** Mk 16:19; Lk 2:11; Mdo 2:23
[c]**5:32** Lk 24:48; Yn 15:26
[d]**5:33** Mdo 2:37; 7:54
[e]**5:34** Mdo 22:3; Lk 2:46; 5:17
[f]**5:36** Mdo 21:38
[g]**5:37** Lk 2:2
[h]**5:38** Lk 15:13
[i]**5:39** 2Nya 13:12; Mdo 11:17
[j]**5:40** Mt 10:17
[k]**5:41** Mt 5:12; Mk 15:21
[l]**5:42** Mdo 2:46; 4:20, 29; 9:22; 13:32
[m]42 *Kristo* maana yake ni *Masiya*, yaani *Aliyetiwa mafuta.*
[n]**6:1** Mdo 2:21; 4:35; 9:29, 39-41; 1Tim 5:3
[o]**6:2** Mdo 11:26; Ebr 4:12; Kut 18:17
[p]**6:3** Mdo 1:14-16; Lk 1:15; Kut 18:21; Neh 13:13; 1Tim 3:7, 8
[q]**6:4** Mdo 2:42
[r]**6:5** Mdo 11:19; 22:20; 8:5-40; 21:8; Lk 1:15
[s]**6:6** Mdo 13:3; 2Tim 1:6; Hes 27; 18; Mk 5:23

7 [a]Neno la Mungu likazidi kuenea. Idadi
ya wanafunzi ikazidi kuongezeka sana
katika Yerusalemu hata makuhani wengi
wakaitii ile imani.

*Kukamatwa Kwa Stefano*

8 [b]Stefano, akiwa amejaa neema na nguvu
za Mungu, alifanya ishara na miujiza
mikubwa miongoni mwa watu. 9 [c]Hata
hivyo, ukainuka upinzani wa watu wa
Sinagogi la Watu Huru (kama lilivyokuwa
linaitwa), la Wayahudi wa Kirene na wa
Iskanderia, na wengine kutoka Kilikia na
Asia. Watu hawa wakaanza kupingana na
Stefano. 10 [d]Lakini hawakuweza kushindana
na hekima yake wala huyo Roho ambaye
alisema kwake.
11 [e]Ndipo kwa siri wakawashawishi watu
fulani waseme, "Tumemsikia Stefano
akisema maneno ya kufuru dhidi ya Mose
na dhidi ya Mungu."

*Stefano Afikishwa Mbele Ya Baraza*

12 [f]Wakawachochea watu, wazee na
walimu wa Sheria, nao wakamkamata
Stefano wakamfikisha mbele ya baraza.
13 [g]Wakaweka mashahidi wa uongo ambao
walishuhudia wakisema, "Mtu huyu kamwe
haachi kusema dhidi ya mahali hapa
patakatifu na dhidi ya Sheria. 14 [h]Kwa
maana tumemsikia akisema kwamba Yesu
wa Nazareti atapaharibu mahali patakatifu
na kubadili desturi zote tulizopewa na
Mose."
15 [i]Watu wote waliokuwa wameketi
katika baraza wakimkazia macho Stefano,
wakaona uso wake unang'aa kama uso wa
malaika.

[a]**6:7** Mdo 12:24; 19:20
[b]**6:8** Yn 4:48
[c]**6:9** Mt 27:32; 22:3; 23:34; 2:9
[d]**6:10** Lk 21:15; Mdo 5:39
[e]**6:11** 2Fal 21:10; Mt 26:59-61
[f]**6:12** Mt 5:22
[g]**6:13** Mt 24:15; Mdo 7:48
[h]**6:14** Mdo 26:3; 28:17
[i]**6:15** Mt 5:22

*Hotuba Ya Stefano*

7 Ndipo kuhani mkuu akamuuliza Stefano,
"Je, mashtaka haya ni ya kweli?"
2 [j]Stefano akajibu, "Ndugu zangu na baba
zangu, nisikilizeni! Mungu wa utukufu
alimtokea baba yetu Abrahamu, alipokuwa
bado yuko Mesopotamia, kabla hajaishi
Harani, 3 [k]akamwambia, 'Ondoka kutoka
nchi yako na kutoka kwa jamii yako, uende
hadi nchi nitakayokuonyesha.'
4 [l]"Hivyo aliondoka katika nchi ya
Wakaldayo akaenda kukaa Harani. Baada
ya kifo cha baba yake, Mungu akamtoa
huko akamleta katika nchi hii ambayo
mnaishi sasa. 5 [m]Mungu hakumpa urithi
wowote katika nchi hii, hakumpa hata
mahali pa kuweka wayo mmoja. Bali Mungu
alimwahidi kuwa yeye na uzao wake baada
yake wangeirithi hii nchi, ingawa wakati
huo Abrahamu hakuwa na mtoto. 6 [n]Mungu
akasema naye hivi: 'Wazao wako watakuwa
wageni kwenye nchi ambayo si yao, nao
watafanywa watumwa na kuteswa kwa
miaka mia nne.' 7 [o]Mungu akasema, 'Lakini
mimi nitaliadhibu taifa watakalolitumikia
kama watumwa, na baadaye watatoka
katika nchi hiyo na wataniabudu mahali
hapa.' 8 [p]Ndipo akampa Abrahamu Agano
la tohara. Naye Abrahamu akamzaa Isaki
na kumtahiri siku ya nane. Baadaye Isaki
akamzaa Yakobo, naye Yakobo akawazaa
wale wazee wetu kumi na wawili.
9 [q]"Kwa sababu wazee wetu walimwonea
wivu Yosefu ndugu yao, walimuuza kama
mtumwa huko Misri. Lakini Mungu alikuwa
pamoja naye. 10 [r]Akamwokoa kutoka
mateso yote yaliyompata, tena akampa
kibali na hekima aliposimama mbele ya
Farao, mfalme wa Misri, ambaye alimweka

[j]**7:2** Za 29:3; Mwa 11:31; 15:7; Mdo 22:1
[k]**7:3** Mwa 12:1-5; 48:4
[l]**7:4** Mwa 12:5; Ebr 11:13
[m]**7:5** Mwa 17:8; 26:3; 12:7; Ebr 11:13
[n]**7:6** Kut 1:8-11; 12:40
[o]**7:7** Mwa 15:13-14; Kut 3:12
[p]**7:8** Mwa 17:9-14; 21:2-4; 29:31-35; 35:16-18, 22-26
[q]**7:9** Mwa 37:4-11; 37:28; 39:2, 21-23; Hag 2:4
[r]**7:10** Mwa 41:37-41; Za 105:20-22

kuwa mtawala juu ya Misri na juu ya jumba
lote la kifalme.
11 [a]“Basi kukawa na njaa katika nchi yote
ya Misri na Kanaani, ikasababisha dhiki
kubwa, nao baba zetu wakawa hawana
chakula. 12 [b]Lakini Yakobo aliposikia
kwamba kuna nafaka huko Misri, aliwatuma
baba zetu, wakaenda huko kwa mara yao
ya kwanza. 13 [c]Walipokwenda mara ya pili,
Yosefu alijitambulisha kwa ndugu zake,
nao ndugu zake Yosefu wakajulishwa kwa
Farao. 14 [d]Ndipo Yosefu akawatuma kumleta
Yakobo baba yake pamoja na jamaa yake
yote, jumla yao walikuwa watu sabini na
watano. 15 [e]Hivyo Yakobo akaenda Misri
ambako yeye na baba zetu walifia. 16 [f]Miili
yao ilirudishwa Shekemu na kuzikwa katika
kaburi ambalo Abrahamu alinunua kutoka
kwa wana wa Hamori kwa kiasi fulani cha
fedha.
17 [g]“Lakini wakati ulipokuwa unakaribia
wa kutimizwa kwa ile ahadi ambayo Mungu
alikuwa amempa Abrahamu, watu wetu
walizidi kuongezeka sana huko Misri.
18 [h]Ndipo mfalme mwingine ambaye
hakujua lolote kuhusu Yosefu akatawala
Misri. 19 [i]Huyu mfalme akawatendea watu
wetu hila na kuwatesa baba zetu kwa
kuwalazimisha wawatupe watoto wao
wachanga ili wafe.
20 [j]“Wakati huo Mose alizaliwa, naye
hakuwa mtoto wa kawaida. Akalelewa
nyumbani kwa baba yake kwa muda wa
miezi mitatu. 21 [k]Waliposhindwa kumficha
zaidi, wakamweka nje mtoni na binti Farao
akamchukua akamtunza kama mtoto wake
mwenyewe. 22 [l]Mose akafundishwa hekima
yote ya Wamisri, akawa mtu hodari kwa
maneno na matendo.

23 [m]“Mose alipokuwa na umri wa miaka
arobaini aliamua kuwatembelea ndugu
zake Waisraeli. 24 Aliona mmoja wao
akidhulumiwa na Mmisri, akamtetea
yule aliyeonewa, akampiga yule Mmisri
akamuua kulipiza kisasi. 25 Mose alidhani
kuwa ndugu zake wangetambua kwamba
Mungu anamtumia ili kuwaokoa, lakini
wao hawakuelewa. 26 [n]Siku iliyofuata Mose
aliwakuta Waisraeli wawili wakigombana,
akajaribu kuwapatanisha kwa kuwaambia,
‘Enyi watu, ninyi ni ndugu, mbona mnataka
kudhulumiana?’
27 [o]“Lakini yule mtu aliyekuwa
akimdhulumu mwenzake akamsukuma
Mose kando, akamuuliza, ‘Ni nani
aliyekufanya mtawala na mwamuzi
juu yetu? 28 Je, unataka kuniua kama
ulivyomuua yule Mmisri jana?’ 29 [p]Mose
aliposikia maneno haya, alikimbilia huko
Midiani alikokaa kama mgeni, naye akapata
watoto wawili wa kiume.
30 [q]“Basi baada ya miaka arobaini kupita,
malaika wa Mungu akamtokea Mose
jangwani karibu na Mlima Sinai katika
kichaka kilichokuwa kinawaka moto.
31 [r]Alipoona mambo haya, alishangaa
yale maono. Aliposogea ili aangalie kwa
karibu, akaisikia sauti ya Bwana, ikisema:
32 [s]‘Mimi ndimi Mungu wa baba zako,
Mungu wa Abrahamu, Isaki na Yakobo.’
Mose alitetemeka kwa hofu na hakuthubutu
kutazama.
33 [t]“Ndipo Bwana akamwambia,
‘Vua viatu vyako kwa maana mahali
unaposimama ni patakatifu. 34 [u]Hakika
nimeona mateso ya watu wangu huko Misri.
Nimesikia kilio chao cha uchungu, nami
nimeshuka ili niwaokoe. Basi sasa njoo,
nami nitakutuma Misri.’

[a]**7:11** Mwa 41:54; 42:5
[b]**7:12** Mwa 42:12
[c]**7:13** Mwa 45:1-4
[d]**7:14** Mwa 45:9-10; Kut 1:5; Kum 10:22
[e]**7:15** Mwa 49:33
[f]**7:16** Mwa 50:13; Yos 24:32
[g]**7:17** Kut 1:6-7; Za 105:24
[h]**7:18** Kut 1:8
[i]**7:19** Kut 1:8-22
[j]**7:20** Kut 2:2; Ebr 11:23
[k]**7:21** Kut 2:3-10
[l]**7:22** 1Fal 4:30; Isa 19:11
[m]**7:23** Kut 2:11; 2:12
[n]**7:26** Kut 2:13
[o]**7:27** Lk 12:14; Mdo 4:7; Mwa 19:9; Hes 16; 13; Kut 2:14
[p]**7:29** Kut 2:11-15
[q]**7:30** Kut 3:2; 2:15, 22; 18:3, 4
[r]**7:31** Kut 3:1-5
[s]**7:32** Mt 22:32; Ebr 11:16; Mdo 3:13; Kut 3:6
[t]**7:33** Kut 3:5-6; Yos 5:15
[u]**7:34** Kut 3:7-10

35 [a]“Huyu ndiye Mose yule waliyemkataa
wakisema, ‘Ni nani aliyekufanya mtawala
na mwamuzi juu yetu?’ Alikuwa ametumwa
na Mungu mwenyewe kuwa mtawala
na mkombozi wao, kwa njia ya yule
malaika aliyemtokea katika kile kichaka.
36 [b]Aliwaongoza wana wa Israeli kutoka
Misri, baada ya kufanya ishara na maajabu
mengi huko Misri, katika Bahari ya Shamu,[c]
na katika jangwa kwa muda wa miaka
arobaini.

37 [d]“Huyu ndiye yule Mose aliyewaambia
Waisraeli, ‘Mungu atawainulia nabii kama
mimi kutoka miongoni mwa ndugu zenu
wenyewe.’ 38 [e]Huyu ndiye yule Mose
aliyekuwa katika kusanyiko huko jangwani,
ambaye malaika alisema naye pamoja
na baba zetu kwenye Mlima Sinai, naye
akapokea maneno yaliyo hai ili atupatie.

39 [f]“Lakini baba zetu walikataa kumtii
Mose, badala yake wakamkataa na kuielekeza
mioyo yao Misri tena. 40 [g]Wakamwambia
Aroni, ‘Tufanyie miungu watakaotuongoza,
kwa maana mtu huyu Mose aliyetutoa nchi
ya Misri, hatujui yaliyompata.’ 41 [h]Huu ni
ule wakati walitengeneza sanamu katika
umbo la ndama, wakailetea sadaka
kufanya maadhimisho kwa ajili ya kile
kitu walichokitengeneza kwa mikono yao
wenyewe. 42 [i]Ndipo Mungu akageuka,
akawaacha waabudu jeshi lote la mbinguni,
kama ilivyoandikwa katika Kitabu cha
Manabii:

“ ‘Je, mliniletea dhabihu na sadaka
kwa miaka arobaini kule
jangwani,
ee nyumba ya Israeli?
43 [j]La, ninyi mliinua madhabahu ya
Moleki,
na nyota ya mungu wenu Refani,
vinyago mlivyotengeneza ili
kuviabudu.
Kwa hiyo nitawapeleka mbali’ kuliko
Babeli.

44 [k]“Baba zetu walikuwa na lile Hema
la Ushuhuda huko jangwani. Lilikuwa
limetengenezwa kama Mungu alivyokuwa
amemwelekeza Mose, kulingana na kielelezo
alichoona. 45 [l]Baba zetu wakiisha kulipokea
hema kwa kupokezana wakiongozwa na
Yoshua katika milki ya nchi kutoka kwa
yale mataifa ambayo Mungu aliyafukuza
mbele yao, nalo likadumu katika nchi
mpaka wakati wa Daudi, 46 [m]ambaye
alipata kibali kwa Mungu, naye akaomba
kwamba ampatie Mungu wa Yakobo
maskani. 47 [n]Lakini alikuwa Solomoni ndiye
alimjengea Mungu nyumba.

48 [o]“Hata hivyo, Yeye Aliye Juu Sana hakai
kwenye nyumba zilizojengwa kwa mikono
ya wanadamu. Kama nabii alivyosema:

49 [p]“ ‘Mbingu ni kiti changu cha enzi,
nayo dunia ni mahali pa kuweka
miguu yangu.
Mtanijengea nyumba ya namna
gani?
asema Bwana.
Au mahali pangu pa kupumzikia
patakuwa wapi?
50 [q]Je, mkono wangu haukufanya vitu
hivi vyote?’

51 [r]“Enyi watu wenye shingo ngumu,
msiotahiriwa mioyo wala masikio, daima
hamwachi kumpinga Roho Mtakatifu, kama
walivyofanya baba zenu. 52 [s]Je, kuna nabii

[a]**7:35** Mdo 7:27; Kut 2:14
[b]**7:36** Kut 12:41; 33; 1; 14:21
[c]36 Yaani Bahari ya Mafunjo.
[d]**7:37** Kum 18:15, 18; Mdo 3:22; Mt 15:5
[e]**7:38** Kut 19:17; Law 27:34; Ebr 4:12; Rum 3:2
[f]**7:39** Hes 14:3-4
[g]**7:40** Kut 32:1-23
[h]**7:41** Za 106:19-20; Ufu 9:20
[i]**7:42** Yos 24:20; Isa 63:19; Yer 19:13
[j]**7:43** Amo 5:25-27
[k]**7:44** Kut 38:21; Hes 17:7; Kut 25:8
[l]**7:45** Yos 23:9; Za 132:1-5
[m]**7:46** 1Fal 8:17; Za 44:2
[n]**7:47** 1Fal 6:1-38; 1Nya 17:12; 2Nya 3:1
[o]**7:48** 1Fal 8:27; 2Nya 2:6
[p]**7:49** Mt 5:32-35; Isa 66:1, 2; Mt 23:22
[q]**7:50** Isa 66:1-2; Lk 23:34
[r]**7:51** Kut 32:9; 33:3-5; Law 26:41; Yer 9:26
[s]**7:52** 2Nya 36:16; Mt 5:12; Mdo 3:14; 1The 2:15

gani ambaye baba zenu hawakumtesa?
Waliwaua wale waliotabiri habari za
kuja kwake yule Mwenye Haki. Nanyi
sasa mmekuwa wasaliti wake na wauaji.
[53] [a]Ninyi ndio mlipokea sheria zilizoletwa
kwenu na malaika, lakini hamkuzitii.”

*Stefano Apigwa Mawe*

[54] [b]Waliposikia haya wakaghadhibika,
wakamsagia meno. [55] [c]Lakini yeye
Stefano, akiwa amejaa Roho Mtakatifu,
alikaza macho mbinguni, akaona utukufu
wa Mungu, na Yesu akiwa amesimama
mkono wa kuume wa Mungu. [56] [d]Akasema,
“Tazameni! Naona mbingu zimefunguka,
na Mwana wa Adamu amesimama upande
wa kuume wa Mungu.”

[57] Lakini wao wakapiga kelele kwa sauti
kubwa, wakaziba masikio yao, wakamrukia
kwa nia moja. [58] [e]Wakamtupa nje ya mji,
wakampiga kwa mawe. Nao mashahidi
wakaweka mavazi yao miguuni mwa kijana
mmoja ambaye jina lake aliitwa Sauli.

[59] [f]Walipokuwa wakimpiga mawe, Stefano
aliomba, “Bwana Yesu, pokea roho yangu.”
[60] [g]Kisha akapiga magoti, akalia kwa sauti
kubwa akasema, “Bwana usiwahesabie
dhambi hii.” Baada ya kusema hayo,
akalala.

8 [h]Naye Sauli alikuwepo pale, akiridhia
kuuawa kwa Stefano.

*Kanisa Lateswa Na Kutawanyika*

Siku ile kukatukia mateso makuu dhidi
ya kanisa huko Yerusalemu, waumini
wote isipokuwa mitume wakatawanyika,
wakakimbilia Uyahudi na Samaria.
[2] [i]Watu wacha Mungu wakamzika Stefano
na kumwombolezea sana. [3] [j]Lakini kwa
habari ya Sauli alikuwa analiharibu kanisa,
akiingia nyumba kwa nyumba, akiwaburuta
wanawake na wanaume na kuwatupa
gerezani.

*Filipo Ahubiri Injili Samaria*

[4] [k]Kwa hiyo wale waliotawanyika
wakalihubiri neno la Mungu kila mahali
walipokwenda. [5] [l]Filipo akateremkia mji
mmoja wa Samaria akawahubiria habari za
Kristo[m] [6] Watu walipomsikia Filipo na kuona
ishara na miujiza aliyofanya, wakasikiliza
kwa bidii yale aliyosema. [7] [n]Pepo wachafu
wakawa wakiwatoka watu wengi huku
wakipiga kelele na wengi waliopooza na
viwete wakaponywa. [8] Hivyo pakawa na
furaha kuu katika mji huo.

*Simoni Mchawi*

[9] [o]Basi mtu mmoja jina lake Simoni
alikuwa amefanya uchawi kwa muda mrefu
katika mji huo akiwashangaza watu wote
wa Samaria. Alijitapa kwamba yeye ni
mtu mkuu, [10] [p]nao watu wote wakubwa
kwa wadogo wakamsikiliza na kumaka,
wakisema “Mtu huyu ndiye uweza wa
Mungu ujulikanao kama ‘Uweza Mkuu.’ ”
[11] Wakamfuata kwa sababu kwa muda
mrefu alikuwa amewashangaza kwa uchawi
wake. [12] [q]Lakini watu walipomwamini Filipo
alipohubiri habari njema za Ufalme wa
Mungu na jina la Yesu Kristo, wakabatizwa
wanaume na wanawake. [13] [r]Simoni naye
akaamini na akabatizwa. Akamfuata Filipo
kila mahali, akistaajabishwa na ishara kuu
na miujiza aliyoiona.

[14] [s]Basi mitume waliokuwa Yerusalemu
waliposikia kuwa Samaria wamelipokea

[a]**7:53** Gal 3:19; Ebr 2:2
[b]**7:54** Mt 5:33; Mdo 5:33
[c]**7:55** Mk 16:19; Mdo 6:5; Lk 22:69
[d]**7:56** Mt 3:16; 8:20; Eze 1:1; Mdo 10:11; Dan 7:13
[e]**7:58** Lk 4:29; Law 24:14-16; Kum 13; 9; Mdo 22:20; 8:1
[f]**7:59** Za 31:5; Lk 23:46
[g]**7:60** Lk 22:41; Mdo 9:40; Mt 5:44
[h]**8:1** Mdo 7:58; 11:19; 9:31
[i]**8:2** Mwa 23:2; 50:10; 2Sam 3:31; Mdo 14:12
[j]**8:3** Flp 3:6; 1Tim 1:13
[k]**8:4** Mdo 15:35; Mt 10:23; Mdo 11:19
[l]**8:5** Mdo 6:5; 21:8
[m]5 *Kristo* maana yake ni *Masiya*, yaani *Aliyetiwa mafuta.*
[n]**8:7** Mk 16:17; Mt 4:24
[o]**8:9** Mdo 13:6; 5:36
[p]**8:10** Mdo 14:11; 28:6
[q]**8:12** Mdo 1:3; 2:38
[r]**8:13** Mdo 19:11
[s]**8:14** Lk 22:8

neno la Mungu, wakawatuma Petro na
Yohana waende huko. 15 [a]Nao walipofika
wakawaombea ili wampokee Roho
Mtakatifu, 16 [b]kwa sababu Roho Mtakatifu
alikuwa bado hajawashukia hata mmoja
ila wamebatizwa tu katika jina la Bwana
Yesu. 17 [c]Ndipo Petro na Yohana wakaweka
mikono yao juu ya wale waliobatizwa, nao
wakapokea Roho Mtakatifu.

18 Simoni alipoona kuwa watu wanapokea
Roho Mtakatifu mitume walipoweka
mikono juu yao, akataka kuwapa fedha
19 akisema, “Nipeni na mimi uwezo huu ili
kila mtu nitakayeweka mikono yangu juu
yake apate kupokea Roho Mtakatifu.”

20 [d]Petro akamjibu, “Fedha yako na
iangamie pamoja nawe, kwa sababu
ulidhani unaweza kununua karama ya
Mungu kwa fedha! 21 [e]Wewe huna sehemu
wala fungu katika huduma hii kwa kuwa
moyo wako si mnyofu mbele za Mungu.
22 [f]Kwa hiyo tubu kwa uovu huu wako
na umwombe Bwana. Yamkini aweza
kukusamehe mawazo uliyo nayo moyoni
mwako. 23 [g]Kwa maana ninaona kwamba
wewe umejawa na uchungu na ni mfungwa
wa dhambi.”

24 [h]Ndipo Simoni akajibu, “Niombeeni
kwa Bwana, ili hayo mliyosema lolote
yasinitukie.”

25 [i]Nao walipokwisha kutoa ushuhuda
na kuhubiri neno la Bwana, wakarudi
Yerusalemu wakihubiri Injili katika vijiji
vingi vya Samaria.

### *Filipo Na Towashi Wa Kushi*

26 [j]Basi malaika wa Bwana akamwambia
Filipo, “Nenda upande wa kusini kwenye ile
barabara itokayo Yerusalemu kuelekea Gaza
ambayo ni jangwa.” 27 [k]Hivyo akaondoka.
Akiwa njiani akakutana na towashi wa
Kushi, aliyekuwa afisa mkuu, mwenye
mamlaka juu ya hazina zote za Kandake,
Malkia wa Kushi. Huyu towashi alikuwa
amekwenda Yerusalemu ili kuabudu,
28 [l]naye akiwa njiani kurudi nyumbani
alikuwa ameketi garini mwake akisoma
kitabu cha nabii Isaya. 29 [m]Roho Mtakatifu
akamwambia Filipo, “Nenda kwenye lile
gari ukae karibu nalo.”

30 Ndipo Filipo akakimbilia lile gari
na kumsikia yule mtu anasoma kitabu
cha nabii Isaya. Filipo akamuuliza, “Je,
unaelewa hayo usomayo?”

31 [n]Yule towashi akasema, “Nitawezaje
kuelewa mtu asiponifafanulia?” Hivyo
akamkaribisha Filipo ili apande na kuketi
pamoja naye.

32 [o]Huyu towashi alikuwa anasoma fungu
hili la Maandiko:

“Aliongozwa kama kondoo aendaye
machinjoni,
kama mwana-kondoo
anyamazavyo
mbele yake yule amkataye manyoya,
hivyo hakufungua kinywa chake.
33 [p]Katika kufedheheshwa kwake
alinyimwa haki yake.
Nani awezaye kueleza juu ya
kizazi chake?
Kwa maana maisha yake
yaliondolewa
kutoka duniani.”

34 Yule towashi akamuuliza Filipo,
“Tafadhali niambie, nabii huyu anena
habari zake mwenyewe au habari za mtu
mwingine?” 35 [q]Ndipo Filipo akaanza
kutumia fungu lile la Maandiko, akamweleza
habari njema za Yesu.

[a]**8:15** Yn 20:22; Mdo 2:38
[b]**8:16** Mdo 10:44; 19:2; Mt 28:19
[c]**8:17** Mdo 6:6
[d]**8:20** Dan 5:17; Mt 10:8
[e]**8:21** Za 78:37
[f]**8:22** Yn 4:40-42
[g]**8:23** Ebr 12:15; Kum 29:18; Isa 58:6
[h]**8:24** 1Fal 13:6; Yer 42:2
[i]**8:25** Mdo 13:48; 8:40
[j]**8:26** Mdo 5:19; 6:5
[k]**8:27** Za 68:31; 87:4; Sef 3:10; Isa 56:3-5; 1Fal 8:41-43; Yn 12:20
[l]**8:28** Za 87:4; Sef 3:10; Isa 56:3-5; 1Fal 8:41-43; Yn 12:20
[m]**8:29** Mdo 20:23; 21:11
[n]**8:31** Yn 16:13
[o]**8:32** Isa 53:7, 8
[p]**8:33** Isa 53:7-8
[q]**8:35** Mt 5:2; Lk 24:27; Mdo 28:23

36 [a]Walipokuwa wakiendelea na safari
wakafika mahali palipokuwa na maji, yule
towashi akamuuliza Filipo, “Tazama, hapa
kuna maji. Kitu gani kitanizuia nisibatizwe?”
[ 37 [b]Filipo akamwambia, “Kama ukiamini
kwa moyo wako wote unaweza kubatizwa.”
Akajibu, “Naamini kuwa Yesu Kristo ni
Mwana wa Mungu.”] 38 Naye akaamuru
lile gari lisimamishwe. Wakateremka
kwenye maji wote wawili, yule towashi
na Filipo, naye Filipo akambatiza. 39 [c]Nao
walipopanda kutoka kwenye maji, ghafula
Roho wa Bwana akamnyakua Filipo, naye
towashi hakumwona tena, lakini akaenda
zake akifurahi. 40 [d]Filipo akajikuta yuko
Azoto, akasafiri akihubiri Injili katika miji
yote mpaka alipofika Kaisaria.

*Kuokoka Kwa Sauli*

**(Matendo 22:6-16; 26:12-18)**

9 [e]Wakati ule ule, Sauli alikuwa bado
anazidisha vitisho vya kuua wanafunzi
wa Bwana, akamwendea kuhani mkuu,
2 [f]naye akamwomba kuhani mkuu ampe
barua za kwenda kwenye masinagogi huko
Dameski, ili akimkuta mtu yeyote wa Njia
Ile, akiwa mwanaume au mwanamke,
aweze kuwafunga na kuwaleta Yerusalemu.
3 [g]Basi akiwa katika safari yake, alipokaribia
Dameski, ghafula nuru kutoka mbinguni
ikamwangaza kotekote. 4 [h]Akaanguka chini,
akasikia sauti ikimwambia, “Sauli, Sauli,
mbona unanitesa?”

5 [i]Sauli akajibu, “U nani wewe, Bwana?”

Ile sauti ikajibu, “Mimi ni Yesu
unayemtesa. 6 [j]Sasa inuka uingie mjini,
nawe utaambiwa yakupasayo kutenda.”

7 [k]Watu waliokuwa wakisafiri pamoja
na Sauli wakasimama bila kuwa na la
kusema, kwa sababu walisikia sauti lakini
hawakumwona aliyekuwa akizungumza.
8 [l]Sauli akainuka kutoka pale chini na
alipojaribu kufungua macho yake hakuweza
kuona kitu chochote. Basi wakamshika
mkono wakamwongoza mpaka Dameski.
9 Naye kwa muda wa siku tatu alikuwa
kipofu naye hakula wala kunywa chochote.

10 [m]Huko Dameski alikuwepo mwanafunzi
mmoja jina lake Anania. Bwana alimwita
katika maono, “Anania!”

Akajibu, “Mimi hapa Bwana.”

11 [n]Bwana akamwambia, “Ondoka uende
katika barabara iitwayo Nyofu ukaulize
katika nyumba ya Yuda mtu kutoka Tarso,
jina lake Sauli, kwa maana wakati huu
anaomba, 12 [o]katika maono amemwona mtu
aitwaye Anania akija na kuweka mikono
juu yake ili apate kuona tena.”

13 [p]Anania akajibu, “Bwana, nimesikia
kutoka kwa watu wengi habari nyingi
kuhusu mtu huyu na madhara yote
aliyowatendea watakatifu wako huko
Yerusalemu. 14 [q]Naye amekuja hapa Dameski
akiwa na mamlaka kutoka kwa viongozi wa
makuhani ili awakamate wote wanaotaja
jina lako.”

15 [r]Lakini Bwana akamwambia Anania,
“Nenda! Mtu huyu ni chombo changu
kiteule nilichokichagua, apate kulichukua
Jina langu kwa watu wa Mataifa na wafalme
wao na mbele ya watu wa Israeli. 16 [s]Nami
nitamwonyesha jinsi impasavyo kuteseka
kwa ajili ya Jina langu.”

17 [t]Kisha Anania akaenda kwenye ile
nyumba, akaingia ndani. Akaweka mikono
yake juu ya Sauli akasema, “Ndugu
Sauli, Bwana Yesu aliyekutokea njiani
amenituma kwako ili upate kuona tena na

[a]**8:36** Mdo 2:38; 10:47
[b]**8:37** Mt 28:19; 16:16; Yn 6:69; 9:35, 38; 11:27; 1Yn 4:15; 5:5, 13
[c]**8:39** 2Fal 2:16; 1The 4:17
[d]**8:40** Mdo 23:23, 33; 25:1-4, 6, 13
[e]**9:1** Mdo 8:3
[f]**9:2** Mdo 22:4; 24:14, 22
[g]**9:3** 1Kor 15:8
[h]**9:4** Isa 6:8; Mt 25:40
[i]**9:5** Mdo 9:16
[j]**9:6** Eze 3:22
[k]**9:7** Yn 12:29; Dan 10:7; Mdo 22:9
[l]**9:8** Mdo 9:18
[m]**9:10** Mdo 12:9; 18:9
[n]**9:11** Mdo 11:25; 21:39
[o]**9:12** Mk 5:23
[p]**9:13** Flp 1:1; Mdo 8:3
[q]**9:14** Mdo 2:21; 9:2, 21
[r]**9:15** Gal 1:15-16; 1Tim 1:12; Efe 3:7-8; Mdo 25:22-23; 26:1
[s]**9:16** 2Kor 11:23-27; 2Tim 1:8
[t]**9:17** Mdo 6:6

ujazwe Roho Mtakatifu.” 18 [a]Ghafula vitu kama magamba vikaanguka chini, kutoka machoni mwa Sauli, akapata kuona tena. Akasimama, akabatizwa. 19 [b]Baada ya kula chakula, akapata nguvu tena. Sauli akakaa siku kadhaa pamoja na wanafunzi huko Dameski.

*Sauli Ahubiri Dameski*

20 [c]Papo hapo akaanza kuhubiri kwenye masinagogi kwamba “Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu” 21 [d]Watu wote waliomsikia Sauli walishangaa na kuuliza, “Huyu si yule mtu aliyesababisha maangamizi makuu huko Yerusalemu miongoni mwa watu waliolitaja jina hili? Naye si amekuja hapa kwa kusudi la kuwakamata na kuwapeleka wakiwa wafungwa mbele ya viongozi wa makuhani?” 22 [e]Sauli akazidi kuwa hodari na kuwashangaza Wayahudi walioishi Dameski kwa kuthibitisha kuwa Yesu ndiye Kristo.[f]

23 [g]Baada ya siku nyingi kupita, Wayahudi wakafanya shauri kumuua Sauli. 24 [h]Lakini shauri lao likajulikana kwa Sauli. Wayahudi wakawa wanalinda malango yote ya mji, usiku na mchana ili wapate kumuua. 25 [i]Lakini wafuasi wake wakamchukua usiku wakamshusha akiwa ndani ya kapu kupitia mahali penye nafasi ukutani.

*Sauli Huko Yerusalemu*

26 [j]Sauli alipofika Yerusalemu akajaribu kujiunga na wanafunzi lakini wote walimwogopa, kwa maana hawakuamini kwamba kweli naye alikuwa mwanafunzi. 27 [k]Lakini Barnaba akamchukua, akampeleka kwa wale mitume. Akawaeleza jinsi Sauli akiwa njiani alivyomwona Bwana, jinsi Bwana alivyosema naye na jinsi alivyohubiri kwa ujasiri kwa jina la Yesu huko Dameski. 28 [l]Kwa hiyo Sauli akakaa nao akitembea kwa uhuru kila mahali huko Yerusalemu, akihubiri kwa ujasiri katika jina la Bwana. 29 [m]Alinena na kuhojiana na Wayahudi wenye asili ya Kiyunani lakini wao walijaribu kumuua. 30 [n]Wale ndugu walipopata habari wakampeleka hadi Kaisaria, wakamsafirisha kwenda Tarso.

31 [o]Ndipo kanisa katika Uyahudi wote, Galilaya na Samaria likafurahia wakati wa amani. Likatiwa nguvu, na kwa faraja ya Roho Mtakatifu, idadi yake ikazidi kuongezeka, na likaendelea kudumu katika kumcha Bwana.

## MATENDO YA PETRO

*(9:32–12:25)*

*Kuponywa Kwa Ainea*

32 [p]Petro alipokuwa akisafiri sehemu mbalimbali, alikwenda kuwatembelea watakatifu walioishi huko Lida. 33 Huko alimkuta mtu mmoja aitwaye Ainea, ambaye alikuwa amepooza na kwa muda wa miaka minane alikuwa hajaondoka kitandani. 34 [q]Petro akamwambia, “Ainea, Yesu Kristo anakuponya, inuka utandike kitanda chako.” Mara Ainea akainuka. 35 [r]Watu wote wa Lida na Sharoni walipomwona Ainea akitembea wakamgeukia Bwana.

*Petro Amfufua Dorkasi*

36 [s]Huko Yafa palikuwa na mwanafunzi jina lake Tabitha (ambalo kwa Kiyunani ni Dorkasi[t]). Huyu alikuwa mkarimu sana, akitenda mema na kuwasaidia

[a]**9:18** Mdo 2:38
[b]**9:19** Mdo 11:26; 26:20
[c]**9:20** Mdo 18:4, 19; 19:8; Mt 4:3
[d]**9:21** Mdo 8:3; Gal 1:13, 23
[e]**9:22** Lk 2:11; Mdo 17:3
[f]22 *Kristo* maana yake ni *Masiya*, yaani *Aliyetiwa mafuta.*
[g]**9:23** Mdo 20:3; 23:12; 25:3
[h]**9:24** Mdo 20:3, 19; 23:16, 30
[i]**9:25** 1Sam 19:12; 2Kor 11:22-33
[j]**9:26** Mdo 26:20; Gal 1:17-18
[k]**9:27** Mdo 4:36; 13:2
[l]**9:28** Gal 1:18
[m]**9:29** Mdo 6:1; 2Kor 11:26
[n]**9:30** Mdo 1:16; 8:40
[o]**9:31** Mdo 8:1
[p]**9:32** Mdo 9:13; 8:14
[q]**9:34** Mdo 3:6, 16; 4:10
[r]**9:35** Wim 2:1; Isa 65:10; Mdo 2:41; 11:21
[s]**9:36** Yn 1:3; Mdo 10:5; 1Tim 2:10; Tit 3:8
[t]36 Tabitha kwa Kiaramu na Dorkasi kwa Kiaramu yote yamaanisha Paa.

maskini. 37 [a]Wakati huo akaugua, akafa na
wakiisha kuuosha mwili wake wakauweka
katika chumba cha ghorofani. 38 [b]Kwa
kuwa Yafa hapakuwa mbali sana na Lida,
wanafunzi waliposikia kwamba Petro yuko
huko waliwatuma watu wawili kwake ili
kumwomba, “Tafadhali njoo huku pasipo
kukawia.”

39 [c]Kwa hiyo Petro akainuka akaenda
nao, naye alipowasili, wakampeleka hadi
kwenye chumba cha ghorofani alipokuwa
amelazwa. Wajane wengi walisimama
karibu naye wakilia na kuonyesha majoho
na nguo nyingine ambazo Dorkasi alikuwa
amewashonea alipokuwa pamoja nao.

40 [d]Petro akawatoa wote nje ya kile
chumba, kisha akapiga magoti akaomba,
akaugeukia ule mwili akasema, “Tabitha,
inuka.” Akafumbua macho yake na
alipomwona Petro, akaketi. 41 [e]Petro
akamshika mkono akamwinua, ndipo
akawaita wale watakatifu na wajane
akamkabidhi kwao akiwa hai. 42 [f]Habari
hizi zikajulikana sehemu zote za Yafa na
watu wengi wakamwamini Bwana. 43 [g]Petro
akakaa Yafa kwa siku nyingi akiishi na
Simoni mtengenezaji ngozi.

### *Kornelio Amwita Petro*

10 [h]Katika mji wa Kaisaria palikuwa
na mtu jina lake Kornelio, ambaye
alikuwa jemadari wa kile kilichojulikana
kama kikosi cha Kiitalia. 2 [i]Yeye alikuwa
mcha Mungu pamoja na wote wa nyumbani
mwake. Aliwapa watu sadaka nyingi na
kumwomba Mungu daima. 3 [j]Siku moja
alasiri, yapata saa tisa, aliona maono
waziwazi, malaika wa Mungu akimjia na
kumwambia, “Kornelio!”

4 [k]Kornelio akamkazia macho kwa hofu
akasema, “Kuna nini, Bwana?”

Malaika akamwambia, “Sala zako na
sadaka zako kwa maskini zimefika juu na
kuwa ukumbusho mbele za Mungu. 5 [l]Sasa
tuma watu waende Yafa wakamwite mtu
mmoja jina lake Simoni aitwaye Petro.
6 [m]Yeye anaishi na Simoni mtengenezaji
ngozi ambaye nyumba yake iko kando ya
bahari.”

7 Yule malaika aliyekuwa akizungumza
naye alipoondoka, Kornelio akawaita
watumishi wake wawili pamoja na askari
mmoja mcha Mungu aliyekuwa miongoni
mwa wale waliomtumikia. 8 [n]Akawaambia
mambo yote yaliyotukia, kisha akawatuma
waende Yafa.

### *Maono Ya Petro*

9 [o]Siku ya pili yake, walipokuwa
wameukaribia mji, wakati wa adhuhuri,
Petro alipanda juu ya nyumba kuomba.
10 [p]Alipokuwa akiomba akahisi njaa,
akatamani kupata chakula. Lakini wakati
walikuwa wakiandaa chakula, akalala
usingizi mzito sana. 11 [q]Akaona mbingu
zimefunguka na kitu kama nguo kubwa
kikishushwa duniani kwa ncha zake
nne. 12 Ndani yake walikuwepo aina zote
za wanyama wenye miguu minne, nao
watambaao nchini, na ndege wa angani.
13 Ndipo sauti ikamwambia “Petro, ondoka,
uchinje na ule.”

14 [r]Petro akajibu, “La hasha Bwana!
Sijawahi kamwe kula kitu chochote kilicho
najisi.”

15 [s]Ile sauti ikasema naye mara ya pili,
“Usikiite najisi kitu chochote Mungu
alichokitakasa.”

16 Jambo hili lilitokea mara tatu na
ghafula ile nguo ikarudishwa mbinguni.

---

[a]**9:37** Mdo 1:13; 20:8
[b]**9:38** Mdo 11:26
[c]**9:39** Mdo 6:1; 1Tim 5:3
[d]**9:40** Mt 9:25; Lk 22:41; Mdo 7:60; Lk 7:14
[e]**9:41** Mdo 9:32
[f]**9:42** Yn 11:45; 12:11
[g]**9:43** Mdo 10:6
[h]**10:1** Mdo 8:40
[i]**10:2** Mdo 13:16-26
[j]**10:3** Mdo 3:1; 9:10; 5:19
[k]**10:4** Za 20:3; Mt 10:42; Ufu 8:4
[l]**10:5** Mdo 9:36
[m]**10:6** Mdo 9:43
[n]**10:8** Mdo 9:36
[o]**10:9** Mt 24:17; Mdo 11:5
[p]**10:10** Mdo 22:17
[q]**10:11** Mdo 11:5-17; Mt 3:16; Ufu 19:11
[r]**10:14** Mdo 9:5; Kum 14:3-20; Eze 4:14
[s]**10:15** Mwa 9:3; Tit 1:15

17 [a]Wakati Petro akiwa bado anajiuliza
kuhusu maana ya maono haya, wale watu
waliokuwa wametumwa na Kornelio
wakaipata nyumba ya Simoni mtengenezaji
wa ngozi wakawa wamesimama mbele ya
lango. 18 Wakabisha hodi na kuuliza kama
Simoni aliyeitwa Petro alikuwa anaishi
hapo.
19 [b]Wakati Petro akiwa anafikiria juu ya
yale maono, Roho Mtakatifu akamwambia,
“Simoni, wako watu watatu wanaokutafuta.
20 [c]Inuka na ushuke, usisite kwenda nao kwa
kuwa mimi nimewatuma.”
21 Petro akashuka na kuwaambia wale
watu waliokuwa wametumwa kutoka kwa
Kornelio, “Mimi ndiye mnayenitafuta.
Mmekuja kwa sababu gani?”
22 [d]Wale watu wakamjibu, “Tumetumwa
na Kornelio yule jemadari. Yeye ni
mtu mwema anayemcha Mungu, na
anaheshimiwa na Wayahudi wote.
Yeye ameagizwa na malaika mtakatifu
akukaribishe nyumbani kwake, ili asikilize
maneno utakayomwambia.” 23 [e]Basi Petro
akawakaribisha wakafuatana naye ndani,
akawapa pa kulala. Kesho yake akaondoka
pamoja nao, na baadhi ya ndugu kutoka
Yafa wakafuatana naye.

### *Petro Nyumbani Mwa Kornelio*

24 [f]Siku iliyofuata wakawasili Kaisaria.
Kornelio alikuwa akiwangoja pamoja na
jamaa yake na marafiki zake wa karibu.
25 Petro alipokuwa akiingia ndani, Kornelio
alikuja kumlaki, akaanguka miguuni pake
kwa heshima. 26 [g]Lakini Petro akamwinua
akamwambia, “Simama, mimi ni
mwanadamu tu.”
27 Petro alipokuwa akizungumza naye
akaingia ndani na kukuta watu wengi
wamekusanyika. 28 [h]Akawaambia, “Mnajua
kabisa kwamba ni kinyume cha sheria
yetu Myahudi kuchangamana na mtu wa
Mataifa au kumtembelea. Lakini Mungu
amenionyesha kwamba nisimwite mtu
yeyote kuwa najisi au asiye safi. 29 Ndiyo
sababu ulipotuma niitwe nilikuja bila
kupinga lolote. Basi sasa naomba unieleze
kwa nini umeniita?”
30 [i]Kornelio akajibu, “Siku nne zilizopita,
nilikuwa nyumbani nikisali saa kama hii,
saa tisa alasiri. Ghafula mtu aliyevaa
nguo zilizong’aa akasimama mbele yangu,
31 [j]akasema, ‘Kornelio, maombi yako
yamesikiwa na sadaka zako kwa maskini
zimekumbukwa mbele za Mungu. 32 Basi
tuma watu waende Yafa wakaulize mtu
mmoja Simoni aitwaye Petro, yeye ni mgeni
katika nyumba ya Simoni mtengenezaji
ngozi, ambaye nyumba yake iko kando ya
bahari.’ 33 Nilituma watu kwako mara moja,
nawe umefanya vyema kuja. Basi sasa sisi
sote tuko hapa mbele za Mungu kuyasikiliza
yote ambayo Bwana amekuamuru
kutuambia.”

### *Hotuba Ya Petro*

34 [k]Ndipo Petro akafungua kinywa
chake akasema, “Mungu hana upendeleo,
35 [l]Lakini katika kila taifa, kila mtu amchaye
na kutenda yaliyo haki hukubaliwa naye.
36 [m]Ninyi mnajua ule ujumbe uliotumwa kwa
Israeli, ukitangaza habari njema za amani
kwa Yesu Kristo. Yeye ni Bwana wa wote.
37 [n]Mnajua yale yaliyotukia katika Uyahudi
wote kuanzia Galilaya baada ya mahubiri
ya Yohana Mbatizaji: 38 [o]Jinsi Mungu
alivyomtia Yesu wa Nazareti mafuta katika
Roho Mtakatifu na jinsi alivyokwenda huku
na huko akitenda mema na kuponya wote
waliokuwa wameonewa na nguvu za ibilisi,
kwa sababu Mungu alikuwa pamoja naye.
39 [p]“Sisi ni mashahidi wa mambo yote
aliyoyafanya katika Uyahudi na Yerusalemu.

---

[a]**10:17** Mdo 9:10; 10:7, 8
[b]**10:19** Mdo 8:29; 13:2; 15:28
[c]**10:20** Mdo 15:7-9
[d]**10:22** Mdo 11:14
[e]**10:23** Mdo 1:16
[f]**10:24** Mdo 8:40
[g]**10:26** Ufu 19:10; 22:8-9
[h]**10:28** Yn 4:9; 18:28; Mdo 15:8-9
[i]**10:30** Mt 28:3; Mk 16:5; Lk 24:4; Yn 20:12
[j]**10:31** Mdo 10:4; Dan 10:12; Ebr 6:10
[k]**10:34** Ay 34:19; Mk 12:14
[l]**10:35** Mdo 15:9
[m]**10:36** Mdo 13:32; Lk 2:14; Mt 28:18
[n]**10:37** Lk 4:14; Mt 4:12-17
[o]**10:38** Mdo 4:26; Mt 4:23; Yn 3:2
[p]**10:39** Lk 24:48; Mdo 5:30

Wakamuua kwa kumtundika msalabani.
40 [a]Lakini Mungu alimfufua kutoka kwa wafu
siku ya tatu na akamwezesha kuonekana
na watu. 41 [b]Hakuonekana kwa watu wote,
lakini kwetu sisi tuliochaguliwa na Mungu
kuwa mashahidi, ambao tulikula na kunywa
naye baada ya kufufuka kwake kutoka kwa
wafu. 42 [c]Naye alituamuru kuhubiri kwa
watu wote na kushuhudia kwamba ndiye
alitiwa mafuta na Mungu kuwa hakimu
wa walio hai na wafu. 43 [d]Manabii wote
walishuhudia juu yake kwamba kila mtu
amwaminiye hupokea msamaha wa dhambi
katika Jina lake.”

### *Watu Wa Mataifa Wapokea Roho Mtakatifu*

44 [e]Wakati Petro alikuwa akisema maneno
haya, Roho Mtakatifu aliwashukia wote
waliokuwa wakisikiliza ule ujumbe.
45 [f]Wale wa tohara walioamini waliokuja
na Petro walishangaa kwa kuona kuwa
kipawa cha Roho Mtakatifu kimemwagwa
juu ya watu wa Mataifa. 46 [g]Kwa kuwa
waliwasikia wakinena kwa lugha mpya na
kumwadhimisha Mungu.

Ndipo Petro akasema, 47 [h]“Je, kuna mtu
yeyote anayeweza kuzuia watu hawa
wasibatizwe kwa maji? Wamempokea
Roho Mtakatifu kama sisi tulivyompokea.”
48 [i]Kwa hiyo akaamuru wabatizwe kwa jina
la Yesu Kristo. Wakamsihi Petro akae nao
kwa siku chache.

### *Petro Aeleza Alivyotumwa Kwa Watu Wa Mataifa*

11 [j]Mitume na ndugu walioamini
waliokuwa huko Uyahudi wakasikia
kuwa watu wa Mataifa nao wamepokea
neno la Mungu. 2 [k]Hivyo Petro alipopanda
Yerusalemu, wale wa tohara waliokuwa
wameamini wakamshutumu, 3 [l]wakisema,
“Ulikwenda kwa watu wasiotahiriwa na
kula pamoja nao.”

4 [m]Ndipo Petro akaanza kuwaeleza kuhusu
mambo yote yalivyotokea hatua kwa hatua
akisema, 5 [n]“Nilikuwa katika mji wa Yafa
nikiomba, nami nikapitiwa na usingizi
wa ghafula, nikaona maono. Kulikuwa na
kitu kama nguo kubwa ikishuka kutoka
mbinguni, ikishushwa kwa ncha zake nne,
nayo ikanikaribia. 6 Nilipoangalia ndani
yake kwa karibu niliona wanyama wenye
miguu minne wa nchini, wanyama wa
mwitu, watambaao na ndege wa angani.
7 Ndipo nikasikia sauti ikiniambia, ‘Petro,
ondoka uchinje na ule.’

8 “Nikajibu, ‘La hasha Bwana! Kitu
chochote kilicho najisi hakijaingia kinywani
mwangu.’

9 [o]“Sauti ikasema kutoka mbinguni mara
ya pili, ‘Usikiite najisi kitu chochote Mungu
alichokitakasa.’ 10 Jambo hili lilitokea
mara tatu, ndipo kile kitu kikavutwa tena
mbinguni.

11 “Wakati ule ule watu watatu,
waliokuwa wametumwa kutoka Kaisaria
waliwasili katika nyumba niliyokuwa
nikikaa. 12 [p]Roho Mtakatifu akaniambia
niende nao bila kuwa na ubaguzi kati yao
na sisi. Hawa ndugu sita pia walifuatana
nami, nasi tukaingia nyumbani mwa huyo
Kornelio. 13 [q]Akatuambia jinsi alivyoona
malaika aliyekuwa amesimama katika
nyumba yake na kusema, ‘Tuma watu
waende Yafa wakamlete Simoni aitwaye
Petro. 14 [r]Yeye atakupa ujumbe ambao kwa
huo wewe na wa nyumbani mwako wote
mtaokoka.’

15 [s]“Nami nilipoanza kusema, Roho
Mtakatifu akashuka juu yao kama vile

[a]**10:40** Mdo 2:24
[b]**10:41** Yn 14:17-22; Lk 24:43; Yn 21:13
[c]**10:42** Mt 28:19-20; 2Tim 4:11; 1Pet 4:5
[d]**10:43** Isa 53:11; Mdo 26:22; 15:9
[e]**10:44** Lk 1:15; Mdo 19:6
[f]**10:45** Mdo 2:33-38; 11:18; 15:8
[g]**10:46** Mk 16:17
[h]**10:47** Mdo 8:36; 11:17; Yn 20:22
[i]**10:48** Mdo 2:38; 8:16
[j]**11:1** Mdo 1:16; Ebr 4:12
[k]**11:2** Mdo 10:45; Gal 2:12
[l]**11:3** Mdo 10:25-28; Gal 2:12
[m]**11:4** Lk 1:3
[n]**11:5** Mdo 10:9-32; 9:10
[o]**11:9** Mdo 10:15
[p]**11:12** Mdo 8:29; 15:9; Rum 3:22; Mdo 1:16; Yn 16:13
[q]**11:13** Mdo 5:19; 10:30
[r]**11:14** Yn 4:53; 1Kor 1:11-16
[s]**11:15** Mdo 10:44; 2:4

alivyotushukia sisi hapo mwanzo. 16 [a]Nami
nikakumbuka neno la Bwana alivyosema,
'Yohana alibatiza kwa maji, lakini ninyi
mtabatizwa katika Roho Mtakatifu.' 17 [b]Basi
ikiwa Mungu aliwapa hawa watu kipawa
kile kile alichotupa sisi tuliomwamini
Bwana Yesu Kristo, mimi ni nani hata
nifikirie kuwa ningeweza kumpinga
Mungu?"
18 [c]Waliposikia haya hawakuwa na la
kupinga zaidi. Nao wakamwadhimisha
Mungu wakisema, "Basi, Mungu amewapa
hata watu wa Mataifa toba iletayo uzima
wa milele."

*Kanisa La Antiokia*

19 [d]Basi wale waliotawanyika kwa ajili ya
mateso yaliyotokana na kifo cha Stefano,
wakasafiri hadi Foinike na Kipro na
Antiokia. Nao hawakuhubiri lile Neno kwa
mtu yeyote isipokuwa Wayahudi. 20 [e]Lakini
baadhi yao walikuwepo watu wa Kipro
na Kirene, ambao walipokuja Antiokia
walinena na Wayunani pia wakiwahubiria
habari njema za Bwana Yesu. 21 [f]Mkono wa
Bwana ulikuwa pamoja nao, nayo idadi
kubwa ya watu wakaamini na kumgeukia
Bwana.
22 [g]Habari hizi zilipofika masikioni mwa
kanisa huko Yerusalemu, wakamtuma
Barnaba aende Antiokia. 23 [h]Alipofika na
kuona madhihirisho ya neema ya Mungu,
akafurahi na kuwatia moyo waendelee
kuwa waaminifu kwa Bwana kwa mioyo
yao yote. 24 [i]Barnaba alikuwa mtu mwema,
aliyejaa Roho Mtakatifu, mwenye imani,
nayo idadi kubwa ya watu wakaongezeka
kwa Bwana.
25 [j]Kisha Barnaba akaenda Tarso
kumtafuta Sauli, 26 [k]naye alipompata
akamleta Antiokia. Hivyo kwa mwaka
mzima Barnaba na Sauli wakakutana na
kanisa na kufundisha idadi kubwa ya
watu. Ilikuwa ni katika kanisa la Antiokia
kwa mara ya kwanza wanafunzi waliitwa
Wakristo.
27 [l]Wakati huo manabii walishuka toka
Yerusalemu hadi Antiokia. 28 [m]Mmoja wao,
jina lake Agabo, akasimama akatabiri
kwa uweza wa Roho Mtakatifu kwamba
njaa kubwa itaenea ulimwengu mzima.
Njaa hiyo ilitokea wakati wa utawala wa
Klaudio. 29 [n]Mitume wakaamua kwamba
kila mtu, kulingana na uwezo alio nao,
atoe msaada kwa ajili ya ndugu wanaoishi
Uyahudi. 30 [o]Wakafanya hivyo, misaada
yao ikapelekwa kwa wazee kwa mikono
ya Barnaba na Sauli.

*Yakobo Auawa, Petro Atiwa Gerezani*

12 [p]Wakati huo huo Mfalme Herode Agripa
aliwakamata baadhi ya watu wa kanisa.
2 [q]Akaamuru Yakobo, ndugu yake Yohana,
auawe kwa upanga. 3 [r]Alipoona jambo hilo
limewapendeza Wayahudi, akaendelea,
akamkamata pia Petro. Hii ilitokea wakati
wa Sikukuu ya Mikate Isiyotiwa Chachu.
4 [s]Baada ya kumkamata alimtia gerezani,
chini ya ulinzi wa vikundi vinne vya askari,
vyenye askari wanne kila kimoja. Herode
alikuwa amekusudia kumtoa na kumfanyia
mashtaka mbele ya watu baada ya Pasaka.
5 [t]Kwa hiyo Petro akawekwa gerezani,
lakini kanisa lilikuwa likimwombea kwa
Mungu kwa bidii.
6 [u]Usiku ule kabla ya siku ambayo Herode

[a]**11:16** Mk 1:8; Mdo 1:5
[b]**11:17** Mdo 10:45-47
[c]**11:18** Rum 10:12-13; 2Kor 7:10
[d]**11:19** Mdo 8:1-4; 14:26; Gal 2:11
[e]**11:20** Mdo 4:36; Mt 27:32; Mdo 4:36; Mt 27:32
[f]**11:21** Lk 1:66; Mdo 2:41-47
[g]**11:22** Mdo 4:36
[h]**11:23** Mdo 15:40; 20:24; 14:22
[i]**11:24** Mdo 2:41; 5:14
[j]**11:25** Mdo 9:11
[k]**11:26** Mdo 6:1-2; 9:19-26; 26:28; 1Pet 4:16
[l]**11:27** 1Kor 11:4; Efe 4:11
[m]**11:28** Mdo 21:10; Mt 24:14; Mdo 18:2
[n]**11:29** Rum 15:26; 2Kor 8:1-4; Mdo 1:16
[o]**11:30** Mdo 14:23; 15:2; 22; 20:17; 1Tim 5:17; Tit 1:5; Yak 5:14; 1Pet 5:1; Mdo 4:36; 12:25
[p]**12:1** Mt 14:1
[q]**12:2** Mt 4:21; Mk 10:39
[r]**12:3** Mdo 24:27; 25:9; Kut 12:15; 23:15; Mdo 20:6
[s]**12:4** Yn 11:15
[t]**12:5** Mdo 1:14; Efe 6:18
[u]**12:6** Mdo 21:33

Agripa alikuwa amekusudia kumtoa na
kumfanyia mashtaka, Petro alikuwa amelala
kati ya askari wawili, akiwa amefungwa
kwa minyororo miwili. Nao walinzi wa
zamu walikuwa wakilinda penye lango
la gereza. 7 [a]Ghafula malaika wa Bwana
akatokea na nuru ikamulika mle ndani
ya gereza. Yule malaika akampiga Petro
ubavuni na kumwamsha, akisema, "Ondoka
upesi!" Mara ile minyororo ikaanguka
kutoka mikononi mwa Petro.
8 Yule malaika akamwambia, "Vaa nguo
zako na viatu vyako." Petro akafanya hivyo.
Kisha akamwambia, "Jifunge vazi lako na
unifuate." 9 [b]Petro akatoka mle gerezani
akiwa amefuatana na yule malaika. Hakujua
wakati huo kuwa yaliyokuwa yakitukia
yalikuwa kweli. Alidhani kuwa anaona
maono. 10 [c]Wakapita lindo la kwanza na la
pili, ndipo wakafika kwenye lango la chuma
linaloelekea mjini. Lango likawafungukia
lenyewe, nao wakapita hapo wakatoka nje.
Baada ya kutembea umbali wa mtaa mmoja,
ghafula yule malaika akamwacha Petro.
11 [d]Ndipo Petro akarudiwa na fahamu,
akasema, "Sasa ninajua bila shaka yoyote
kuwa Bwana amemtuma malaika wake
na kuniokoa kutoka makucha ya Herode
Agripa na kutoka matazamio yote ya
Wayahudi."
12 [e]Mara Petro alipotambua hili alikwenda
nyumbani kwa Maria, mama yake Yohana
aliyeitwa pia Marko, ambako watu wengi
walikuwa wamekutana kwa maombi.
13 [f]Petro alipobisha hodi kwenye lango
la nje, mtumishi wa kike jina lake Roda,
akaja kumfungulia. 14 [g]Alipoitambua
sauti ya Petro, alifurahi mno akarudi bila
kufungua na kuwaeleza kwamba, "Petro
yuko langoni!"
15 [h]Wakamwambia yule mtumishi wa kike,
"Umerukwa na akili." Alipozidi kusisitiza
kuwa ni kweli, wakasema, "Lazima awe ni
malaika wake."
16 Lakini Petro aliendelea kugonga
langoni, nao walipofungua lango na
kumwona Petro, walistaajabu sana. 17 [i]Yeye
akawaashiria kwa mkono wake wanyamaze
kimya, akawaeleza jinsi Bwana alivyomtoa
gerezani. Naye akaongeza kusema,
"Waelezeni Yakobo na ndugu wengine
habari hizi." Kisha akaondoka akaenda
sehemu nyingine.
18 [j]Kulipokucha kukawa na fadhaa
kubwa miongoni mwa wale askari kuhusu
yaliyomtukia Petro. 19 [k]Baada ya Herode
kuamuru atafutwe kila mahali na bila
kumpata, aliwahoji wale askari walinzi
kisha akatoa amri wauawe. Basi Herode
Agripa akatoka Uyahudi akaenda Kaisaria,
akakaa huko kwa muda.

*Kifo Cha Herode Agripa*

20 [l]Basi Herode Agripa alikuwa
amekasirishwa sana na watu wa Tiro na
Sidoni. Hivyo watu wa miji hiyo miwili
wakaungana pamoja wakatafuta kukutana
naye. Wakiisha kuungwa mkono na Blasto,
mtumishi maalum wa Mfalme Herode
Agripa aliyeaminika, wakaomba mapatano
ya amani maana nchi zao zilitegemea
nchi ya huyo mfalme kwa mahitaji yao ya
chakula.
21 Katika siku iliyochaguliwa Herode
Agripa akavaa mavazi yake ya kifalme,
akaketi kwenye kiti chake cha enzi na
kuwahutubia watu. 22 [m]Watu waliokuwa
wamekusanyika wakapiga kelele,
wakisema, "Hii si sauti ya mwanadamu,
bali ni ya Mungu." 23 [n]Ghafula, kwa kuwa
Herode hakumpa Mungu utukufu, malaika

---

[a]**12:7** Mdo 5:19; Za 107:14; Mdo 16:26
[b]**12:9** Mdo 9:10
[c]**12:10** Mdo 5:19; 16:26
[d]**12:11** Lk 15:17; Za 34:7; Dan 3:28; 6:22; 2Kor 11:10; 2Pet 2:9
[e]**12:12** Mdo 12:25; 15:37; Kol 4:10; 2Tim 4:11; 1Pet 5:13
[f]**12:13** Yn 18:16
[g]**12:14** Lk 24:41
[h]**12:15** Mt 18:10
[i]**12:17** Mdo 19:33; 21:40
[j]**12:18** Mdo 5:21, 22
[k]**12:19** Mdo 8:1-4; 16:27; 8:40
[l]**12:20** Mt 11:21; 1Fal 5:9, 11; Eze 27:17
[m]**12:22** Eze 28:2
[n]**12:23** Mdo 5:19; 1Sam 25:38; 2Sam 24:16; 2Fal 19:35

wa Bwana akampiga, naye akaliwa na
chango, akafa.
24 [a]Lakini neno la Mungu likaendelea
mbele na kuenea, nao wengi wakaambatana
nalo.
25 [b]Barnaba na Sauli walipomaliza ile
huduma yao iliyowapeleka, wakarudi
Yerusalemu wakiwa pamoja na Yohana
aitwaye Marko.

## SAFARI YA KWANZA YA PAULO KUENEZA INJILI

*(13:1–14:28)*

### *Barnaba Na Sauli Wanatumwa*

1 [c]Katika kanisa huko Antiokia ya Shamu
walikuwako manabii na walimu, yaani:
Barnaba, Simeoni aitwaye Nigeri, Lukio
Mkirene, Manaeni aliyekuwa amelelewa
pamoja na Mfalme Herode Agripa, na
Sauli. 2 [d]Walipokuwa wakimwabudu Bwana
na kufunga, Roho Mtakatifu akasema,
"Nitengeeni Sauli na Barnaba kwa kazi ile
maalum niliyowaitia." 3 [e]Ndipo baada ya
kufunga na kuomba, wakawawekea mikono
yao na wakawatuma waende zao.

### *Barnaba Na Sauli Waenda Kipro*

4 [f]Hivyo, wakiwa wametumwa na Roho
Mtakatifu, wakashuka kwenda Seleukia na
kutoka huko wakasafiri baharini mpaka
kisiwa cha Kipro. 5 [g]Walipowasili katika
mji wa Salami, wakahubiri neno la Mungu
katika sinagogi la Wayahudi. Pia walikuwa
na Yohana Marko kuwa msaidizi wao.
6 [h]Walipokwisha kupita katika nchi zote
hizo wakafika Pafo, ambapo walikutana
na Myahudi mmoja mchawi aliyekuwa
nabii wa uongo, jina lake Bar-Yesu. 7 [i]Mtu
huyu alikuwa pamoja na Sergio Paulo,
mtu mwenye hekima aliyekuwa msaidizi
wa mwakilishi wa mtawala wa kile kisiwa.
Sergio Paulo akawaita Sauli na Barnaba
akitaka kusikia neno la Mungu. 8 [j]Lakini
Elima yule mchawi (hii ndiyo maana ya
jina lake), aliwapinga Barnaba na Sauli na
kujaribu kumpotosha yule mkuu wa kile
kisiwa aiache imani. 9 [k]Ndipo Sauli, ambaye
pia aliitwa Paulo, akiwa amejawa na Roho
Mtakatifu, akamkazia macho Elima huyo
mchawi, 10 [l]akamwambia, "Ewe mwana
wa ibilisi, wewe ni adui wa kila kilicho
haki! Umejaa kila aina ya udanganyifu na
ulaghai. Je, hutaacha kuzipotosha njia za
Bwana zilizonyooka? 11 [m]Nawe sasa sikiliza,
mkono wa Bwana u dhidi yako. Utakuwa
kipofu, wala hutaona jua kwa muda."
Mara ukungu na giza vikamfunika, naye
akaenda huku na huko akitafuta mtu wa
kumshika mkono ili amwonyeshe njia.
12 [n]Yule mkuu wa kile kisiwa alipoona
yaliyotukia, akaamini kwa sababu
alistaajabishwa na mafundisho kuhusu
Bwana.

### *Paulo Na Barnaba Huko Antiokia Ya Pisidia*

13 [o]Kisha Paulo na wenzake wakasafiri
toka Pafo wakafika Perga huko Pamfilia.
Lakini, Yohana Marko akawaacha huko,
akarejea Yerusalemu. 14 [p]Kutoka Perga
wakaendelea hadi Antiokia ya Pisidia. Siku
ya Sabato wakaingia ndani ya sinagogi,
wakaketi. 15 [q]Baada ya Sheria ya Mose na
Kitabu cha Manabii kusomwa, viongozi wa
sinagogi wakawatumia ujumbe wakisema,
"Ndugu, kama mna neno la kuwafariji watu
hawa, tafadhali lisemeni."
16 [r]Paulo akasimama, akawapungia mkono
na kusema: "Enyi wanaume wa Israeli na

---

[a]**12:24** Ebr 4:12; Mdo 6:7; 19:20
[b]**12:25** Mdo 4:36; 11:30; 12:12
[c]**13:1** Mdo 11:19, 27; Efe 4:11; Mdo 4:36; Mt 27:32; 14:1
[d]**13:2** Mdo 8:29; 14:26; 9:15; 22:21
[e]**13:3** Mdo 6:6; 14:26; 1Tim 4:14; 5:22
[f]**13:4** Mdo 13:2, 3; 4:36; 15:39
[g]**13:5** Ebr 4:12; 9:20; 12:12
[h]**13:6** Mdo 8:9; Mt 7:15
[i]**13:7** Mdo 13:8, 12; 18:12; 19:38
[j]**13:8** Mdo 8:9; Isa 30:11; Mdo 6:7; 2Tim 3:8
[k]**13:9** Lk 1; 15
[l]**13:10** Mt 13:38; Yn 8:44; Hos 14:9
[m]**13:11** Kut 9:3; 1Sam 5:6, 7; Za 32:4; Mwa 19:10, 11
[n]**13:12** Mdo 13:7
[o]**13:13** Mdo 13:6; 2:10; 12:12
[p]**13:14** Mdo 14:19, 21; 13:27, 42, 44; 16:13; 18:4; 9:20
[q]**13:15** Mdo 15:21; Lk 4:16; Ebr 13:22
[r]**13:16** Mdo 12:17; 10:35

ninyi nyote mnaomcha Mungu. 17 [a]Mungu
wa watu hawa wa Israeli aliwachagua baba
zetu, akawafanya kustawi walipokuwa huko
Misri, kwa uwezo mwingi akawaongoza na
kuwatoa katika nchi ile. 18 [b]Kwa muda wa
miaka arobaini alivumilia matendo yao
walipokuwa jangwani. 19 [c]Naye baada ya
kuyaangamiza mataifa saba waliokuwa
wakiishi katika nchi ya Kanaani, akawapa
Waisraeli nchi yao iwe urithi wao. 20 [d]Haya
yote yalichukua kama muda wa miaka 450.

“Baada ya haya, Mungu akawapa waamuzi
mpaka wakati wa nabii Samweli. 21 [e]Ndipo
watu wakaomba wapewe mfalme, naye
Mungu akawapa Sauli mwana wa Kishi wa
kabila la Benyamini, aliyetawala kwa miaka
arobaini. 22 [f]Baada ya kumwondoa Sauli
katika ufalme, akawainulia Daudi kuwa
mfalme wao. Mungu pia alimshuhudia,
akisema, ‘Nimemwona Daudi mwana wa
Yese, mtu anayeupendeza moyo wangu,
atakayetimiza mapenzi yangu yote.’

23 [g]“Kutoka uzao wa mtu huyu, Mungu
amewaletea Israeli Mwokozi Yesu, kama
alivyoahidi. 24 [h]Kabla ya kuja kwa Yesu,
Yohana alihubiri toba na ubatizo kwa
watu wote wa Israeli. 25 [i]Yohana alipokuwa
anakamilisha kazi yake, alisema: ‘Ninyi
mnadhani mimi ni nani? Mimi si yeye.
La hasha, lakini yeye yuaja baada yangu,
ambaye mimi sistahili kufungua kamba za
viatu vya miguu yake.’

26 [j]“Ndugu zangu, wana wa Abrahamu,
nanyi watu wa Mataifa mnaomcha Mungu,
ujumbe huu wa wokovu umeletwa kwetu.
27 [k]Kwa sababu wakaao Yerusalemu na
viongozi wao hawakumtambua wala
kuelewa maneno ya manabii yasomwayo
kila Sabato, bali waliyatimiza maneno
hayo kwa kumhukumu yeye. 28 [l]Ijapokuwa
hawakupata sababu yoyote ya kumhukumu
kifo, walimwomba Pilato aamuru auawe.
29 [m]Walipokwisha kufanya yale yote
yaliyoandikwa kumhusu, walimshusha
kutoka msalabani na kumzika kaburini.
30 [n]Lakini Mungu alimfufua kutoka kwa
wafu. 31 [o]Naye kwa siku nyingi akawatokea
wale waliokuwa pamoja naye kuanzia
Galilaya hadi Yerusalemu. Nao sasa
wamekuwa mashahidi wake kwa watu
wetu.

32 [p]“Nasi tunawaletea habari njema,
kwamba yale Mungu aliyowaahidi baba
zetu 33 [q]sasa ameyatimiza kwetu sisi
watoto wao, kwa kumfufua Yesu, kama
ilivyoandikwa katika Zaburi ya pili:

“ ‘Wewe ni Mwanangu;
leo mimi nimekuzaa.’

34 [r]Kwa kuwa Mungu alimfufua kutoka kwa
wafu asioze kamwe, alitamka maneno haya:

“ ‘Nitakupa wewe baraka takatifu
zilizo za hakika
nilizomwahidi Daudi.’

35 [s]Kama ilivyosemwa mahali pengine
katika Zaburi,

“ ‘Hutamwacha Aliye Mtakatifu wako
kuona uharibifu.’

36 [t]“Kwa maana Daudi akiisha kulitumikia
kusudi la Mungu katika kizazi chake,
alilala; akazikwa pamoja na baba zake na
mwili wake ukaoza. 37 [u]Lakini yule ambaye

---

[a]**13:17** Kut 6:6, 7; Kum 7:6-8
[b]**13:18** Kum 1:31; Hes 14:33; Za 95:10; Mdo 7:36
[c]**13:19** Kum 7:1; Yos 14:2; Za 78:55
[d]**13:20** Amu 2:17; 1Sam 3:19, 20; Mdo 3:24
[e]**13:21** 1Sam 8:5, 19; 10:1; 9:1, 2
[f]**13:22** 1Sam 15:23, 26; 16:13; Za 89:20; Yer 3:15; Isa 44:28; 1Sam 13:14
[g]**13:23** Mt 1:1; Lk 2:11; Mt 1:21; 2Sam 7:11; 22:51; Yer 30:9
[h]**13:24** Mk 1:4; Lk 3:3
[i]**13:25** Mdo 20:24; Yn 1:20; Mt 3:11; Yn 1:27
[j]**13:26** Mdo 22:5; Lk 3:8; Mt 4:12; Mdo 28:28; Mt 10:6
[k]**13:27** Mdo 3:17; Lk 24:27; Mt 1:22
[l]**13:28** Mt 27:20-25; Mdo 3:13
[m]**13:29** Mt 1:22; Lk 8:31; Mdo 5:30; Lk 23:53
[n]**13:30** Mt 16:21; 28:6; Mdo 2:24
[o]**13:31** Mt 28; 16; Lk 24:48
[p]**13:32** Isa 40:9; 52:7; Mdo 5:42; 8:35; 10:36; Rum 12; 4:13; 9:4
[q]**13:33** Mdo 2:24; Za 2:7; Mt 3:17
[r]**13:34** Isa 55:6; 55:3
[s]**13:35** Za 16; 10; Mdo 2:27
[t]**13:36** Mt 9:24; 2Sam 7:12; 1Fal 2:10; 2Nya 29:28; Mdo 2:29
[u]**13:37** Mdo 2:24

Mungu alimfufua kutoka kwa wafu hakuona
uharibifu.
38 [a]“Kwa hiyo ndugu zangu, nataka ninyi
mjue kwamba kwa kupitia huyu Yesu
msamaha wa dhambi unatangazwa kwenu.
39 [b]Kwa kupitia yeye, kila mtu amwaminiye
anahesabiwa haki kwa kila kitu ambacho
asingeweza kuhesabiwa haki kwa sheria
ya Mose. 40 [c]Kwa hiyo jihadharini ili yale
waliyosema manabii yasiwapate:

41 [d]“ ‘Angalieni, enyi wenye dhihaka,
mkastaajabu, mkaangamie,
kwa maana nitatenda jambo wakati
wenu
ambalo hamtasadiki,
hata kama mtu akiwaambia.’ ”

42 [e]Paulo na Barnaba walipokuwa
wakitoka nje ya sinagogi, watu
wakawaomba wazungumze tena mambo
hayo Sabato iliyofuata. 43 [f]Baada ya
kusanyiko la Sinagogi kutawanyika, wengi
wa Wayahudi na waongofu wa dini ya
Kiyahudi wakawafuata Paulo na Barnaba,
wakazungumza nao na kuwahimiza
wadumu katika neema ya Mungu.
44 Sabato iliyofuata, karibu watu wote
wa mji walikuja kusikiliza neno la Bwana.
45 [g]Lakini Wayahudi walipoona ule umati
mkubwa wa watu walijawa na wivu,
wakayakanusha maneno Paulo aliyokuwa
akisema.
46 [h]Ndipo Paulo na Barnaba wakawajibu
kwa ujasiri, wakisema, “Ilitupasa kunena
nanyi neno la Mungu kwanza. Lakini kwa
kuwa mmelikataa, mkajihukumu wenyewe
kuwa hamstahili uzima wa milele, sasa
tunawageukia watu wa Mataifa. 47 [i]Kwa
maana hili ndilo Bwana alilotuamuru:

“ ‘Nimewafanya ninyi kuwa nuru
kwa watu wa Mataifa,
ili mpate kuuleta wokovu hadi
miisho ya dunia.’ ”

48 [j]Watu wa Mataifa waliposikia haya
wakafurahi na kulitukuza neno la Bwana;
nao wote waliokuwa wamekusudiwa uzima
wa milele wakaamini.
49 [k]Neno la Bwana likaenea katika eneo lile
lote. 50 [l]Lakini Wayahudi wakawachochea
wanawake wenye kumcha Mungu, wenye
vyeo pamoja na watu maarufu katika mji,
wakachochea mateso dhidi ya Paulo na
Barnaba na kuwafukuza kutoka eneo hilo.
51 [m]Hivyo Paulo na Barnaba wakakung’uta
mavumbi ya miguu yao ili kuwapinga, nao
wakaenda Ikonio. 52 [n]Wanafunzi wakajawa
na furaha na Roho Mtakatifu.

### *Paulo Na Barnaba Huko Ikonio*

14 [o]Huko Ikonio Paulo na Barnaba
waliingia pamoja katika sinagogi la
Wayahudi kama ilivyokuwa desturi yao.
Huko wakahubiri kwa uwezo mkubwa kiasi
kwamba Wayahudi pamoja na watu wa
Mataifa wakaamini. 2 [p]Lakini wale Wayahudi
waliokataa kuamini, wakawachochea watu
wa Mataifa, wakatia chuki ndani ya mioyo
yao dhidi ya wale walioamini. 3 [q]Hivyo
Paulo na Barnaba wakakaa huko kwa muda
wa kutosha wakihubiri kwa ujasiri juu ya
Bwana, ambaye alithibitisha ujumbe wa
neema yake kwa kuwawezesha kufanya
ishara na miujiza. 4 [r]Lakini watu wa mji ule
waligawanyika, wengine wakakubaliana na
Wayahudi na wengine na mitume. 5 [s]Watu
wa Mataifa na Wayahudi wakajiunga na
baadhi ya viongozi, wakafanya mpango wa
kuwatendea mitume mabaya na kuwapiga

[a]**13:38** Lk 24:47; Mdo 2:38
[b]**13:39** Yn 3:15; Rum 3:28; 10:4
[c]**13:40** Hab 1:4
[d]**13:41** Hab 1:5
[e]**13:42** Mdo 13:14
[f]**13:43** Mdo 11:23; 14:22; Rum 3:24
[g]**13:45** Mdo 18:6; 1Pet 4:4; 1The 2:16
[h]**13:46** Mdo 13:26; 3:26; 18:6; 22:21; 26:20; 28:28; Rum 11:11; Mt 21:41
[i]**13:47** Lk 2:32; Isa 49:6
[j]**13:48** Mdo 13:49; 8:25; Rum 8:29
[k]**13:49** Mdo 13:48
[l]**13:50** 1The 2:16
[m]**13:51** Mt 10:14; Mdo 14:1; 19:21; 2Tim 3:11
[n]**13:52** Mdo 11:26; Lk 1:5
[o]**14:1** Mdo 13:51; 9:20; 2:41
[p]**14:2** Mdo 4:29; Yn 4:48; Ebr 2:4
[q]**14:3** Mt 10:23
[r]**14:4** Mdo 16:10; 13:32
[s]**14:5** Mdo 20:3; 14:19; 2Tim 3:11

mawe. 6 [a]Lakini mitume walipopata habari
hizi wakakimbilia Listra na Derbe, miji ya
Likaonia na sehemu zilizopakana nayo.
7 [b]Huko wakaendelea kuhubiri habari
njema.

*Paulo Na Barnaba Huko Listra*

8 [c]Katika mji wa Listra, alikuwako
kiwete, ambaye alikuwa amelemaa tangu
kuzaliwa na hakuwa ametembea kamwe.
9 [d]Alimsikiliza Paulo alipokuwa akihubiri.
Paulo alipomtazama akaona ana imani
ya kuponywa. 10 [e]Paulo akapaza sauti,
"Simama kwa miguu yako!" Mara yule mtu
akasimama upesi akaanza kutembea!

11 [f]Ule umati wa watu ulipoona yaliyokuwa
yamefanywa na Paulo, wakapiga kelele
kwa lugha yao ya Kilikaonia wakasema,
"Miungu imetushukia katika umbo la
binadamu!" 12 [g]Wakamwita Barnaba Zeu na
Paulo wakamwita Herme kwa kuwa ndiye
alikuwa msemaji mkuu. 13 [h]Kuhani wa Zeu,
ambaye hekalu lake lilikuwa nje kidogo tu
ya mji, akaleta mafahali na mashada ya
maua penye lango la mji kwa sababu yeye
na ule umati wa watu walitaka kuwatolea
dhabihu.

14 [i]Lakini mitume Paulo na Barnaba
waliposikia haya, wakararua nguo zao,
wakawaendea wale watu kwa haraka,
wakawapigia kelele, wakisema, 15 [j]"Enyi
watu, kwa nini mnafanya mambo
haya? Sisi ni wanadamu tu kama ninyi!
Tunawaletea habari njema, tukiwaambia
kwamba mgeuke mtoke katika mambo haya
yasiyofaa, mmwelekee Mungu aliye hai,
aliyeziumba mbingu na nchi na bahari na
vitu vyote vilivyomo. 16 [k]Zamani aliwaachia
mataifa waishi walivyotaka. 17 [l]Lakini
hakuacha kuwaonyesha watu uwepo wake:
Ameonyesha wema kwa kuwanyeshea
mvua toka mbinguni na kuwapa mazao kwa
majira yake, naye amewapa chakula tele na
kuijaza mioyo yenu na furaha." 18 Hata kwa
maneno haya yote, ilikuwa vigumu kuuzuia
ule umati wa watu kuwatolea dhabihu.

19 [m]Ndipo wakaja baadhi ya Wayahudi
kutoka Antiokia na Ikonio wakawashawishi
wale watu, wakampiga Paulo kwa mawe,
wakamburuta hadi nje ya mji, wakidhani
amekufa. 20 [n]Lakini baada ya wanafunzi
kukusanyika akainuka na kurudi mjini.
Kesho yake yeye na Barnaba wakaondoka
kwenda Derbe.

*Paulo Na Barnaba Warudi Antiokia Huko Syria*

21 [o]Wakahubiri habari njema katika mji
huo na kupata wanafunzi wengi. Kisha
wakarudi Listra, Ikonio na Antiokia,
22 [p]wakiwaimarisha wanafunzi na kuwatia
moyo waendelee kudumu katika imani.
Wakawaonya wakisema, "Imetupasa
kuingia katika Ufalme wa Mungu kwa
kupitia katika taabu nyingi." 23 [q]Nao baada
ya kuwateua wazee katika kila kanisa, kwa
kufunga na kuomba wakawakabidhi kwa
Bwana waliyemwamini. 24 [r]Kisha wakapitia
Pisidia wakafika Pamfilia. 25 Baada ya
kuhubiri neno la Mungu huko Perga,
wakateremkia Atalia.

26 [s]Kutoka Atalia wakasafiri baharini
wakarudi Antiokia, ambako walikuwa
wamesifiwa kwa ajili ya neema ya Mungu
kutokana na ile huduma waliyokuwa
wameikamilisha. 27 [t]Walipowasili Antiokia
wakaliita kanisa pamoja na kutoa taarifa
ya yale yote Mungu aliyokuwa ametenda

[a]**14:6** Mt 10:23
[b]**14:7** Mdo 16:10; 13:32
[c]**14:8** Mdo 3:2
[d]**14:9** Mt 9:28-29; 13:58
[e]**14:10** Mdo 3:8
[f]**14:11** Mdo 10:26; Yak 5:17; Mdo 13:32; 1Sam 12:2
[g]**14:12** Kut 7:1
[h]**14:13** Dan 2:46
[i]**14:14** Mt 26:65; Mk 14:63
[j]**14:15** Mdo 10:26; 13:32; 1Sam 12:21; Mt 16:16; Mwa 1:1
[k]**14:16** Mdo 17:30; Za 81:12; Mk 4:5
[l]**14:17** Mdo 17:27; Rum 1:20; Ay 5:10; Za 65:10
[m]**14:19** Mdo 13:45; 13:51; 2Kor 11:25; 2Tim 3:11
[n]**14:20** Mdo 11:26
[o]**14:21** Mdo 13:51
[p]**14:22** Mdo 11:23; 13:43; 2Tim 3:12
[q]**14:23** Mdo 11:30; Tit 1:5; Mdo 13:3; 20:32
[r]**14:24** Mdo 2:10
[s]**14:26** Mdo 11:19; 11:23; 15:40; 13:13
[t]**14:27** Mdo 15:4-12; 21:19; Kol 4:3; Ufu 3:8

kupitia kwao na jinsi alivyokuwa amefungua
mlango wa imani kwa ajili ya watu wa
Mataifa. 28 Nao wakakaa huko pamoja na
wanafunzi kwa muda mrefu.

*Baraza La Yerusalemu*

15 [a]Baadhi ya watu wakashuka Antiokia
kutoka Uyahudi, nao wakawa
wanawafundisha wandugu: “Msipotahiriwa
kufuatana na desturi aliyofundisha Mose,
hamwezi kuokoka.” 2 [b]Baada ya Paulo
na Barnaba kutokubaliana nao kukawa
na mabishano makali, Paulo na Barnaba
na baadhi ya wengine miongoni mwao
wakachaguliwa kwenda Yerusalemu ili
kujadiliana jambo hili na mitume na
wazee. 3 [c]Hivyo wakasafirishwa na kanisa,
wakiwa njiani wakapitia nchi ya Foinike
na Samaria, wakawaeleza jinsi watu
wa Mataifa walivyookoka. Habari hizi
zikaleta furaha kubwa kwa ndugu wote.
4 [d]Walipofika Yerusalemu, walipokelewa na
kanisa na mitume pamoja na wazee, ndipo
Paulo na Barnaba wakawaarifu kila kitu
Mungu alichokuwa amefanya kupitia kwao.
5 [e]Ndipo baadhi ya walioamini wa
madhehebu ya Mafarisayo wakasimama
na kusema, “Hao watu wa Mataifa lazima
watahiriwe na waagizwe kutii sheria ya
Mose.”
6 Mitume na wazee wakakutana pamoja ili
kufikiri jambo hili. 7 [f]Baada ya majadiliano
mengi, Petro akasimama na kusema, “Ndugu
zangu, mnajua kwamba siku za kwanza
Mungu alinichagua ili kwa midomo yangu
watu wa Mataifa wapate kusikia ujumbe
wa Injili na kuamini. 8 [g]Mungu, yeye ajuaye
mioyo, alionyesha kwamba anawakubali
kwa kuwapa Roho Mtakatifu kama vile
alivyotupa sisi. 9 [h]Mungu hakutofautisha
kati yetu na wao, bali alitakasa mioyo yao
kwa imani. 10 [i]Sasa basi, mbona mnataka
kumjaribu Mungu kwa kuweka kongwa
shingoni mwa wanafunzi ambalo baba zetu
wala sisi hatukuweza kulibeba? 11 [j]Lakini
sisi tunaamini ya kuwa tunaokolewa kwa
neema ya Bwana Yesu Kristo, kama wao
wanavyookolewa.”
12 [k]Kusanyiko lote likakaa kimya,
wakawasikiliza Paulo na Barnaba wakieleza
jinsi Mungu alivyowatumia kutenda
ishara na maajabu kwa watu wa Mataifa.
13 [l]Walipomaliza kunena, Yakobo akasema,
“Ndugu zangu, nisikilizeni. 14 [m]Simoni
amekwisha kutueleza jinsi Mungu, kwa
mara ya kwanza alivyoonyesha kuhusika
kwa kujichagulia watu kutoka watu wa
Mataifa kwa ajili ya Jina lake. 15 [n]Maneno
ya manabii yanakubaliana na jambo hili,
kama ilivyoandikwa:

16 [o]“ ‘Baada ya mambo haya nitarudi,
nami nitajenga upya
nyumba ya Daudi iliyoanguka.
Nitajenga tena magofu yake
na kuisimamisha,
17 [p]ili wanadamu wengine wote
wapate kumtafuta Bwana,
hata wale watu wa Mataifa wote
ambao wanaitwa kwa Jina langu,
asema Bwana, afanyaye mambo
haya’
18 [q]ambayo yamejulikana tangu
zamani.

19 [r]“Kwa hivyo uamuzi wangu ni
kwamba, tusiwataabishe watu wa Mataifa
wanaomgeukia Mungu. 20 [s]Badala yake,
tuwaandikie kwamba wajiepushe na
vyakula vilivyonajisiwa kwa kutolewa
sanamu, wajiepushe na uasherati, au kula

[a]**15:1** Gal 2:12; 5:2, 3; Mdo 6:14
[b]**15:2** Gal 2:2; Mdo 11:30
[c]**15:3** Mdo 14:27
[d]**15:4** Mdo 21:19
[e]**15:5** Mdo 5:17; Mt 3:7; Mdo 15:1
[f]**15:7** Mdo 10:20; 11:12; 10:1-48
[g]**15:8** Mdo 1:24; Ufu 2:23; Mdo 10:44, 47
[h]**15:9** Mdo 10:28, 34; 11:12; 10:43
[i]**15:10** Mt 23:4; Gal 5:1
[j]**15:11** Gal 2:16; Efe 2:5-8
[k]**15:12** Yn 4:48; Mdo 14:27; 21:19
[l]**15:13** 1Kor 15:7; Gal 1:19
[m]**15:14** 2Pet 1:1; Mdo 15:7; Lk 1:68
[n]**15:15** Amo 9:11-12
[o]**15:16** Amo 9:11-12
[p]**15:17** Amo 9:11, 12
[q]**15:18** Isa 45:21
[r]**15:19** Mdo 15:28; 1The 1:9
[s]**15:20** 1Kor 8:7-13; Ufu 2:14, 20; 1Kor 10:7-8; Ufu 2:14; 20; Mwa 9:4; Law 7:26

mnyama aliyenyongwa, na damu. 21 [a]Kwa maana katika kila mji kwa vizazi vilivyopita, Mose amekuwa na wale wanaotangaza sheria yake kwa kuwa imekuwa ikisomwa kwa sauti kubwa katika masinagogi kila Sabato."

*Barua Kwa Waumini Wa Mataifa*

22 [b]Mitume na wazee pamoja na kanisa lote, wakaamua kuwachagua baadhi ya watu wao na kuwatuma Antiokia pamoja na Paulo na Barnaba. Wakamchagua Yuda aitwaye Barsaba pamoja na Sila, watu wawili waliokuwa viongozi miongoni mwa ndugu. 23 [c]Wakatumwa na barua ifuatayo:

> Sisi mitume na wazee, ndugu zenu,
>
> Kwa ndugu Mataifa mlioamini mlioko Antiokia, Shamu na Kilikia:
>
> Salamu.
>
> 24 [d]Tumesikia kwamba kuna baadhi ya watu waliokuja huko kutoka kwetu bila ruhusa yetu na kuwasumbua, wakiyataabisha mawazo yenu. 25 Hivyo tumekubaliana wote kuwachagua baadhi ya watu na kuwatuma kwenu pamoja na wapendwa wetu Barnaba na Paulo, 26 [e]watu ambao wamehatarisha maisha yao kwa ajili ya jina la Bwana wetu Yesu Kristo. 27 [f]Kwa hiyo tunawatuma Yuda na Sila, kuthibitisha kwa maneno ya mdomo mambo haya tunayowaandikia. 28 [g]Kwa maana imempendeza Roho Mtakatifu na sisi tusiwatwike mzigo wowote mkubwa zaidi ya mambo haya yafuatayo ambayo ni ya lazima: 29 [h]Kwamba mjiepushe na vyakula vilivyotolewa sadaka kwa sanamu, na damu, au kula nyama ya mnyama aliyenyongwa, na mjiepushe na uasherati. Mkiyaepuka mambo haya, mtakuwa mmefanya vyema.
>
> Kwaherini.

30 Hivyo wakaagwa, wakashuka kwenda Antiokia. Baada ya kulikusanya kanisa pamoja, wakawapa ile barua. 31 Nao hao watu wakiisha kuisoma, wakafurahishwa sana kwa ujumbe wake wa kutia moyo. 32 [i]Yuda na Sila, ambao wenyewe walikuwa manabii, wakanena maneno mengi ya kuwatia moyo na kuwajenga katika imani wale ndugu walioamini. 33 [j]Baada ya kukaa huko Antiokia kwa muda, wakaagwa kwa amani na wale ndugu ili waende kwa wale waliowatuma. [ 34 [k]Lakini Sila bado akaendelea kukaa huko.] 35 [l]Lakini Paulo na Barnaba walibaki Antiokia ambako wao pamoja na wengine wengi walifundisha na kuhubiri neno la Bwana.

## SAFARI YA PILI YA PAULO KUENEZA INJILI

*(15:36–18:22)*

*Paulo Na Barnaba Wagawanyika*

36 [m]Baada ya muda, Paulo akamwambia Barnaba, "Turudi tukawatembelee ndugu katika miji yote tuliyohubiri neno la Bwana tuone jinsi wanavyoendelea." 37 [n]Barnaba alitaka wamchukue Yohana aitwaye Marko waende naye. 38 [o]Lakini Paulo aliona si vyema kwa sababu aliwahi kuwaacha walipokuwa huko Pamfilia, hakutaka kuendelea kufanya kazi naye. 39 Pakatokea ubishi mkali kati ya Paulo na Barnaba kuhusu jambo hili, hivyo wakagawanyika. Barnaba akamchukua Yohana Marko wakasafiri baharini kwenda Kipro. 40 [p]Lakini Paulo akamchagua Sila na akaondoka baada ya ndugu kuwatakia

[a]**15:21** Mdo 13:15; 2Kor 3:14-15
[b]**15:22** Mdo 11:30; 16:19, 25, 26; 2Kor 1:19; 1The 1:1; 1Pet 5:12
[c]**15:23** Mdo 20:23
[d]**15:24** Mdo 15:1; Gal 1:7; 5:10
[e]**15:26** Mdo 11:19; 11:23; 15:40; 13:13
[f]**15:27** Mdo 15:22
[g]**15:28** Mdo 5:32
[h]**15:29** Mdo 21:25
[i]**15:32** Mdo 14:22; 18:23
[j]**15:33** 1Sam 1:17; Lk 7:50
[k]**15:34** Mdo 4:36; 13:40
[l]**15:35** Mdo 8:4
[m]**15:36** Mdo 13:4, 13, 14, 51; 14:1, 6, 24; 25
[n]**15:37** Mdo 12:12
[o]**15:38** Mdo 13:13
[p]**15:40** Mdo 11:23; 15:41; Lk 2:2; Mdo 6:9; 16:5

neema ya Bwana. 41 Akapitia Shamu na
Kilikia, akiimarisha makanisa ya huko.

*Timotheo Aungana Na Paulo Na Sila*

16 [a]Paulo akafika Derbe na kisha Listra,
ambako kulikuwa na mwanafunzi
mmoja jina lake Timotheo, ambaye mama
yake alikuwa Myahudi aliyeamini, lakini
baba yake alikuwa Myunani. 2 [b]Alikuwa
amesifiwa sana na wale ndugu waliokuwa
wameamini huko Listra na Ikonio 3 [c]Paulo
alitaka Timotheo afuatane naye, hivyo
akamchukua na kumtahiri kwa sababu ya
Wayahudi waliokuwa wanaishi eneo lile
kwa maana wote walimjua baba yake ni
Myunani. 4 [d]Walipokuwa wakienda mji
kwa mji, wakawa wanawapa maamuzi
yaliyotolewa na mitume na wazee huko
Yerusalemu ili wayafuate. 5 [e]Hivyo
makanisa yakawa imara katika imani na
kuongezeka kiidadi kila siku.

6 [f]Paulo pamoja na wenzake wakasafiri
sehemu za Frigia na Galatia, kwa kuwa
Roho Mtakatifu hakuwaruhusu kulihubiri
neno huko Asia. 7 [g]Walipofika mpaka wa
Misia, wakajaribu kuingia Bithinia lakini
Roho wa Yesu hakuwaruhusu. 8 [h]Kwa hiyo
wakapita Misia, wakafika Troa. 9 [i]Wakati
wa usiku Paulo akaona maono, mtu wa
Makedonia amesimama akimsihi, "Vuka
uje huku Makedonia utusaidie." 10 [j]Baada
ya Paulo kuona maono haya, tulijiandaa
kwa haraka kuondoka kwenda Makedonia
tukiwa tumesadiki kuwa Mungu alikuwa
ametuita kuhubiri habari njema huko.

*Kuokoka Kwa Lidia*

11 [k]Tukasafiri kwa njia ya bahari kutoka
Troa na kwenda moja kwa moja hadi
Samothrake, kesho yake tukafika Neapoli.
12 [l]Kutoka huko tukasafiri hadi Filipi,
mji mkuu wa jimbo hilo la Makedonia,
uliokuwa koloni ya Warumi. Nasi tukakaa
huko siku kadhaa.

13 [m]Siku ya Sabato tukaenda nje ya lango
la mji kando ya mto, mahali ambapo
tulitarajia tungepata mahali pa kufanyia
maombi. Tukaketi, tukaanza kuongea
na baadhi ya wanawake waliokuwa
wamekusanyika huko. 14 [n]Mmoja wa wale
wanawake waliotusikiliza aliitwa Lidia,
mfanyabiashara wa nguo za zambarau,
mwenyeji wa mji wa Thiatira, aliyekuwa
mcha Mungu. Bwana akaufungua moyo
wake akaupokea ujumbe wa Paulo. 15 [o]Basi
alipokwisha kubatizwa yeye na watu wa
nyumba yake, alitukaribisha nyumbani
kwake akisema, "Kama mmeona kweli
mimi nimemwamini Bwana, karibuni mkae
nyumbani mwangu." Naye akatushawishi.

*Paulo Na Sila Watiwa Gerezani*

16 [p]Siku moja, tulipokuwa tukienda
mahali pa kusali, tulikutana na mtumwa
mmoja wa kike ambaye alikuwa na
pepo wa uaguzi. Naye alikuwa amewapa
mabwana zake mapato makubwa ya fedha
kwa ubashiri. 17 [q]Huyu msichana alikuwa
akimfuata Paulo na sisi akipiga kelele,
"Watu hawa ni watumishi wa Mungu Aliye
Juu Sana, wao wanawatangazieni njia ya
wokovu." 18 [r]Akaendelea kufanya hivi kwa
siku nyingi, lakini Paulo akiwa ameudhika
sana, akageuka na kumwambia yule pepo
mchafu, "Ninakuamuru katika jina la
Yesu Kristo, umtoke!" Yule pepo mchafu
akamtoka saa ile ile.

19 [s]Basi mabwana wa yule mtumwa
wa kike walipoona kuwa tumaini lao la
kuendelea kujipatia fedha limetoweka,

[a]**16:1** Mdo 14; 6; Rum 16:21; Flp 1:1; Mdo 14:6; 1Kor 4:17; 16:10; 2Kor 1:1; Flp 1:1
[b]**16:2** Mdo 1:16; 13:51; 16:40; 1:16; 13:51
[c]**16:3** Gal 2:3
[d]**16:4** Mdo 11:30; 15:2; 15:28, 29
[e]**16:5** Mdo 9:31; 15:41
[f]**16:6** Mdo 18; 23; Gal 1:2; 3:1; Mdo 2:9
[g]**16:7** Flp 1:19; 1Pet 1:11
[h]**16:8** 2Kor 2:12; 2Tim 4:12
[i]**16:9** Mdo 9:10; 20:1
[j]**16:10** Mdo 20:11-38
[k]**16:11** Mdo 16:8
[l]**16:12** Flp 1:1; 1The 2:2
[m]**16:13** Mdo 13:14
[n]**16:14** Ufu 1:1; Lk 24:45
[o]**16:15** Mdo 11:14
[p]**16:16** Kum 18:11; 1Sam 28:3-7
[q]**16:17** Mk 5:7; 15:17
[r]**16:18** Mk 16:17; 1:25
[s]**16:19** Mdo 19:25, 26; 15:22; 21:30; Yak 2:6

wakawakamata Paulo na Sila wakawaburuta
mpaka sokoni mbele ya viongozi wa
mji. 20 [a]Baada ya kuwafikisha mbele ya
mahakimu wakawashtaki wakisema, “Hawa
watu wanaleta ghasia katika mji wetu, nao
ni Wayahudi. 21 [b]Wanafundisha desturi
ambazo sisi raiya wa Kirumi hatuwezi
kuzikubali au kuzitimiza.”

22 [c]Umati wa watu waliokuwepo
wakajiunga katika kuwashambulia Paulo
na Sila na wale mahakimu wakaamuru
wavuliwe nguo zao na wachapwe viboko.
23 [d]Baada ya kuwachapa sana, wakawatupa
gerezani na kumwagiza mkuu wa gereza
awalinde kikamilifu. 24 [e]Kufuata maelekezo
haya, yule mkuu wa gereza akawaweka
katika chumba cha ndani sana mle gerezani,
na akawafunga miguu yao kwa minyororo.

25 [f]Ilipokaribia usiku wa manane, Paulo
na Sila walikuwa wakiomba na kuimba
nyimbo za kumsifu Mungu, nao wafungwa
wengine walikuwa wakiwasikiliza.
26 [g]Ghafula pakatokea tetemeko kubwa la
ardhi, hata msingi wa gereza ukatikisika.
Mara milango ya gereza ikafunguka na
ile minyororo iliyowafunga kila mmoja
ikafunguka. 27 [h]Yule mkuu wa gereza
alipoamka na kuona milango ya gereza
iko wazi, akachomoa upanga wake akataka
kujiua, akidhani ya kuwa wafungwa wote
wametoroka. 28 Lakini Paulo akapiga kelele
kwa sauti kubwa, akasema, “Usijidhuru kwa
maana sisi sote tuko hapa!”

29 Yule askari wa gereza akaagiza taa
ziletwe, akaingia ndani ya kile chumba
cha gereza, akapiga magoti akitetemeka
mbele ya Paulo na Sila. 30 [i]Kisha akawaleta
nje akisema, “Bwana zangu, nifanye nini
nipate kuokoka?”

31 [j]Wakamjibu, “Mwamini Bwana Yesu
Kristo, nawe utaokoka, pamoja na watu
wa nyumbani mwako.” 32 Wakamwambia
neno la Bwana yeye pamoja na wote
waliokuwako nyumbani mwake. 33 [k]Wakati
ule ule, yule mkuu wa gereza akawachukua,
akawaosha majeraha yao, kisha akabatizwa
yeye pamoja na wote waliokuwa nyumbani
mwake bila kuchelewa. 34 [l]Akawapandisha
nyumbani mwake akawaandalia chakula,
yeye pamoja na nyumba yake yote
wakafurahi sana kwa kuwa sasa walikuwa
wamemwamini Mungu.

35 Kulipopambazuka wale mahakimu
wakawatuma maafisa wao kwa mkuu
wa gereza wakiwa na agizo linalosema,
“Wafungue wale watu, waache waende
zao.” 36 [m]Mkuu wa gereza akamwambia
Paulo “Mahakimu wameagiza niwaache
huru, kwa hiyo tokeni na mwende zenu
kwa amani.”

37 [n]Lakini Paulo akawaambia wale
maafisa, “Wametupiga hadharani bila
kutufanyia mashtaka na kutuhoji, nao
wakatutupa gerezani, hata ingawa sisi ni
raiya wa Rumi. Nao sasa wanataka kututoa
gerezani kwa siri? Hapana! Wao na waje
wenyewe watutoe humu gerezani.”

38 [o]Wale maafisa wakarudi na kuwaambia
wale mahakimu maneno haya, wakaogopa
sana walipofahamu kuwa Paulo na Sila
ni raiya wa Rumi. 39 [p]Kwa hiyo wakaja
wakawaomba msamaha, wakawatoa
gerezani, wakawaomba waondoke katika
ule mji. 40 [q]Baada ya Paulo na Sila kutoka
gerezani walikwenda nyumbani kwa
Lidia, ambapo walikutana na wale ndugu
walioamini, wakawatia moyo, ndipo
wakaondoka.

*Ghasia Huko Thesalonike*

17 [r]Wakasafiri kupitia Amfipoli na
Apolonia wakafika Thesalonike,

[a]**16:20** Mdo 17:16
[b]**16:21** Es 3:8
[c]**16:22** 2Kor 11:25; 1The 2:2
[d]**16:23** Mdo 16:27, 36
[e]**16:24** Ay 33:11; Yer 29:26
[f]**16:25** Efe 5:19
[g]**16:26** Mdo 4:31; 12:10; 12:7
[h]**16:27** Mdo 11:14
[i]**16:30** Mdo 2:37; 9:6; Lk 3:10
[j]**16:31** Yn 3:16, 36; 6:47; 1Yn 5:10
[k]**16:33** Mdo 16:25; 2:38
[l]**16:34** Mdo 11:14
[m]**16:36** Mdo 15:33
[n]**16:37** Mdo 22:25-29
[o]**16:38** Mdo 22:29
[p]**16:39** Mt 8:34
[q]**16:40** Mdo 1:16
[r]**17:1** 2The 1:1; 2Tim 4:10

ambako kulikuwa na sinagogi la Wayahudi.
2 Kama desturi yake, Paulo aliingia ndani
ya sinagogi, na kwa muda wa Sabato tatu
akawa anahojiana nao kutoka kwenye
Maandiko, 3 [ab]akidhihirisha wazi na
kuthibitisha kwamba ilikuwa lazima
Kristo[c] ateswe na afufuke kutoka kwa wafu.
Akasema, "Huyu Yesu ninayewaambia
habari zake, ndiye Kristo." 4 [d]Baadhi ya
Wayahudi wakasadiki, wakaungana na
Paulo na Sila, wakiwepo idadi kubwa ya
Wayunani waliomcha Mungu na wanawake
wengi mashuhuri.
5 [e]Lakini Wayahudi ambao hawakuwa
wameamini wakawa na wivu, wakawakodi
watu waovu kutoka sokoni, wakakutanisha
umati wa watu, wakaanzisha ghasia mjini.
Wakaenda mbio nyumbani kwa Yasoni
wakiwatafuta Paulo na Sila ili kuwaleta
nje penye ule umati wa watu. 6 [f]Lakini
walipowakosa wakamburuta Yasoni na
ndugu wengine mbele ya maafisa wa mji,
wakipiga kelele: "Watu hawa ni wale
walioupindua ulimwengu wamekuja huku,
7 [g]naye Yasoni amewakaribisha nyumbani
mwake. Hawa wote wanaasi amri za Kaisari
wakisema yuko mfalme mwingine aitwaye
Yesu." 8 Waliposikia haya, ule umati wa
watu na maafisa wa mji wakaongeza ghasia.
9 [h]Nao baada ya kuchukua dhamana kwa
ajili ya Yasoni na wenzake wakawaacha
waende zao.

### *Paulo Na Sila Huko Beroya*

10 [i]Usiku ule ule, wale ndugu walioamini
wakawapeleka Paulo na Sila waende zao
Beroya. Walipowasili huko wakaenda
kwenye sinagogi la Wayahudi. 11 [j]Hawa
Waberoya walikuwa waungwana zaidi
kuliko wale wa Thesalonike, kwa kuwa
waliupokea ule ujumbe kwa shauku kubwa
na kuyachunguza Maandiko kila siku ili
kuona kama yale Paulo aliyosema yalikuwa
kweli. 12 [k]Wayahudi wengi wakaamini
pamoja na wanawake na wanaume wa
Kiyunani wa tabaka la juu.
13 [l]Lakini wale Wayahudi wa Thesalonike
waliposikia kuwa Paulo anahubiri neno
la Mungu huko Beroya, wakaenda huko
ili kuwashawishi watu na kuwachochea.
14 [m]Mara hiyo, wale ndugu wakamsafirisha
Paulo hadi pwani, lakini Sila na Timotheo
wakabaki Beroya. 15 [n]Wale waliomsindikiza
Paulo wakaenda naye mpaka Athene, kisha
wakarudi Beroya wakiwa na maagizo
kutoka kwa Paulo kuhusu Sila na Timotheo
kwamba wamfuate upesi iwezekanavyo.

### *Paulo Huko Athene*

16 [o]Paulo alipokuwa akiwasubiri huko
Athene, alisumbuka sana moyoni mwake
kuona vile mji huo ulivyojaa sanamu.
17 [p]Hivyo akahojiana kwenye sinagogi na
Wayahudi pamoja na Wayunani waliomcha
Mungu, na pia sokoni kila siku na watu
aliopatana nao huko. 18 [q]Kisha baadhi ya
Waepikureo na Wastoiko wenye falsafa
wakakutana naye. Baadhi yao wakasema,
"Je, huyu mpayukaji anajaribu kusema
nini?" Wengine wakasema, "Inaonekana
anasema habari za miungu ya kigeni."
Walisema haya kwa sababu Paulo alikuwa
anahubiri habari njema kuhusu Yesu na
ufufuo wa wafu. 19 [r]Hivyo wakamchukua
na kumleta kwenye mkutano wa Areopago,
walikomwambia, "Je, tunaweza kujua
mafundisho haya mapya unayofundisha
ni nini? 20 Wewe unaleta mambo mapya
masikioni mwetu, hivyo tungetaka kujua

---

[a]**17:3** Mdo 9:20; 13:14; 8:35; 18:28
[b]**17:3** Lk 24:26; Mdo 3:18; Lk 24:46; Mdo 2:24; 9; 22; 18:28
[c]3 *Kristo* maana yake ni *Masiya*, yaani *Aliyetiwa mafuta.*
[d]**17:4** Mdo 15:22
[e]**17:5** 1The 2:16; Rum 16:21
[f]**17:6** Mdo 16:19; Mt 24:14; Mdo 16:20
[g]**17:7** Lk 23:2; Yn 19:12
[h]**17:9** Mdo 17:5
[i]**17:10** Mdo 20:4
[j]**17:11** Lk 16:29; Yn 5:39
[k]**17:12** Mdo 2:41
[l]**17:13** Ebr 4:12; 1The 2:14
[m]**17:14** Mdo 15:22; 16:1
[n]**17:15** Mdo 18:1; 1The 3:1; Mdo 18:5
[o]**17:16** 2Pet 2:8
[p]**17:17** Mdo 9:20
[q]**17:18** Mdo 4:2
[r]**17:19** Mk 1:27

maana yake ni nini.” 21 [a](Waathene na
wageni wote walioishi humo hawakutumia
muda wao kufanya chochote kingine
isipokuwa kueleza au kusikia mambo
mapya).
22 [b]Ndipo Paulo akasimama katikati ya
Areopago akasema, “Enyi watu wa Athene!
Ninaona kwamba katika kila jambo ninyi ni
watu wa dini sana. 23 [c]Kwa kuwa nilipokuwa
nikitembea mjini na kuangalia kwa bidii
vitu vyenu vya kuabudiwa, niliona huko
madhabahu moja iliyoandikwa: KWA
MUNGU ASIYEJULIKANA. Basi sasa kile
ambacho mmekuwa mkikiabudu kama
kisichojulikana, ndicho ninachowahubiria.
24 [d]“Mungu aliyeumba dunia na vyote
vilivyomo ndani yake, yeye ndiye
Bwana wa mbingu na nchi, hakai katika
mahekalu yaliyojengwa kwa mikono ya
wanadamu. 25 [e]Wala hatumikiwi na mikono
ya wanadamu kana kwamba anahitaji
chochote, kwa sababu yeye mwenyewe
ndiye awapaye watu wote uhai na pumzi
na vitu vyote. 26 [f]Kutoka kwa mtu mmoja,
yeye aliumba mataifa yote ya wanadamu
ili waikalie dunia yote, naye akaweka
nyakati za kuishi. 27 [g]Mungu alifanya
hivyo ili wanadamu wamtafute na huenda
wakamfikia ingawa kwa kupapasapapasa
ijapokuwa kwa kweli hakai mbali na kila
mmoja wetu. 28 [h]‘Kwa kuwa katika yeye
tunaishi, tunatembea na kuwa na uzima
wetu.’ Kama baadhi ya watunga mashairi
wenu walivyosema, ‘Sisi ni watoto wake.’
29 [i]“Kwa kuwa sisi ni watoto wa Mungu,
haitupasi kudhani kuwa uungu ni kama
sanamu ya dhahabu au ya fedha au ya
jiwe, mfano uliotengenezwa kwa ubunifu
na ustadi wa mwanadamu. 30 [j]Zamani
wakati wa ujinga, Mungu alijifanya kama
haoni, lakini sasa anawaamuru watu wote
kila mahali watubu. 31 [k]Kwa kuwa ameweka
siku ambayo atauhukumu ulimwengu
kwa haki akimtumia mtu aliyemchagua.
Amewahakikishia watu wote mambo haya
kwa kumfufua Kristo kutoka kwa wafu.”
32 [l]Waliposikia habari za ufufuo wa wafu,
baadhi yao wakadhihaki, lakini wengine
wakasema, “Tunataka kukusikia tena
ukizungumza juu ya jambo hili.” 33 Kwa hiyo
Paulo akaondoka katikati yao. 34 [m]Lakini
baadhi yao wakaungana naye wakaamini.
Kati yao alikuwepo Dionisio, Mwareopago
na mwanamke mmoja aliyeitwa Damari na
wengine wengi.

*Paulo Huko Korintho*

18 [n]Baada ya haya, Paulo akaondoka
Athene akaenda Korintho. 2 [o]Huko
akakutana na Myahudi mmoja jina lake
Akila, mwenyeji wa Ponto, ambaye alikuwa
amewasili karibuni kutoka Italia pamoja na
mkewe Prisila, kwa sababu Klaudio alikuwa
ameamuru Wayahudi wote waondoke
Rumi. Paulo akaenda kuwaona, 3 [p]naye kwa
kuwa alikuwa mtengeneza mahema kama
wao, akakaa na kufanya kazi pamoja nao.
4 [q]Kila Sabato Paulo alikuwa akihojiana nao
katika sinagogi, akijitahidi kuwashawishi
Wayahudi na Wayunani.
5 [r]Sila na Timotheo walipowasili kutoka
Makedonia, walimkuta Paulo akiwa
amejitolea muda wake wote katika kuhubiri,
akiwashuhudia Wayahudi kwamba Yesu
ndiye Kristo[s] 6 [t]Wayahudi walipompinga

[a]**17:21** Mdo 17:15
[b]**17:22** Mdo 17:16, 19
[c]**17:23** Yn 4:22
[d]**17:24** Isa 42:5; Mdo 14:15; Isa 66:1-2; Mt 11:25; Mdo 7:48
[e]**17:25** Za 50:10-12; Isa 42:5
[f]**17:26** Kum 32:8; Ay 12:23
[g]**17:27** Isa 55:6; Mdo 14:17
[h]**17:28** Kum 30:20; Ay 12:10
[i]**17:29** Isa 40:18-20; Rum 3:25; 1Pet 1:14; Lk 24:47
[j]**17:30** Mdo 14:16; Rum 3:25; 1Pet 1:14; Lk 24:47
[k]**17:31** Mt 10:15; Za 96; 13; 98:9; Tit 2:11, 12
[l]**17:32** Mdo 17:18, 31
[m]**17:34** Mdo 17:19; 22
[n]**18:1** Mdo 17:15; 1Kor 1:2
[o]**18:2** Rum 16:3; 2Tim 4:19; Mdo 11:28
[p]**18:3** 1The 2:9; 2The 3:8
[q]**18:4** Mdo 13:14
[r]**18:5** Mdo 15:22; 16:1; 16:9; 17:14-15; 9:22; 17:3
[s]5 *Kristo* maana yake ni *Masiya*, yaani *Aliyetiwa mafuta.*
[t]**18:6** Mdo 13:35; 2Sam 1:16; Eze 18:13

Paulo na kukufuru, yeye aliyakung’uta
mavazi yake, akawaambia, “Damu yenu
na iwe juu ya vichwa vyenu! Mimi sina
hatia, nimetimiza wajibu wangu. Kuanzia
sasa nitawaendea watu wa Mataifa.”
7 [a]Kisha akaondoka mle kwenye sinagogi,
akaenda nyumbani kwa mtu mmoja jina
lake Tito Yusto, aliyekuwa mcha Mungu.
Nyumba yake ilikuwa karibu na sinagogi.
8 [b]Kiongozi wa hilo sinagogi, aliyeitwa
Krispo, akamwamini Bwana, yeye pamoja
na watu wote wa nyumbani mwake. Nao
Wakorintho wengi waliomsikia Paulo pia
wakaamini na kubatizwa.
9 [c]Usiku mmoja Bwana akamwambia
Paulo katika maono, “Usiogope, lakini
endelea kusema wala usinyamaze, 10 [d]kwa
maana mimi niko pamoja nawe, wala
hakuna mtu atakayeweza kukushambulia
ili kukudhuru, kwa kuwa ninao watu wengi
katika mji huu ambao ni watu wangu.”
11 [e]Hivyo Paulo akakaa huko kwa muda
wa mwaka mmoja na nusu, akiwafundisha
neno la Mungu.
12 [f]Lakini wakati Galio alipokuwa
msaidizi wa mwakilishi wa mtawala
huko Akaya, Wayahudi waliungana
kumshambulia Paulo, wakamkamata na
kumpeleka mahakamani. 13 Wakamshtaki
wakisema, “Mtu huyu anawashawishi watu
wamwabudu Mungu kinyume cha sheria.”
14 [g]Paulo alipotaka kujitetea, Galio
akawaambia Wayahudi, “Kama ninyi
Wayahudi mlikuwa mkilalamika kuhusu
makosa makubwa ya uhalifu ingekuwa
haki kwangu kuwasikiliza. 15 [h]Lakini kwa
kuwa linahusu maneno, majina na sheria
yenu, amueni ninyi wenyewe. Mimi
sitakuwa mwamuzi wa mambo haya.”
16 Akawafukuza kutoka mahakamani.
17 [i]Ndipo wote wakamkamata Sosthene
kiongozi wa sinagogi, wakampiga mbele
ya mahakama, lakini Galio hakujali kitendo
chao hata kidogo.

### *Paulo Arudi Antiokia*

18 [j]Baada ya kukaa Korintho kwa muda,
Paulo akaagana na wale ndugu walioamini,
akasafiri kwa njia ya bahari kwenda Shamu
akiwa amefuatana na Prisila na Akila.
Walipofika Kenkrea, Paulo alinyoa nywele
zake kwa kuwa alikuwa ameweka nadhiri.
19 [k]Walipofika Efeso, Paulo aliwaacha
Prisila na Akila huko, lakini yeye akaingia
kwenye sinagogi akawa anajadiliana na
Wayahudi. 20 Walipomwomba akae nao kwa
muda mrefu zaidi hakukubali. 21 [l]Lakini
alipokuwa akiondoka, akaahidi, “Nitarudi
kama Mungu akipenda.” Kisha akasafiri
kwa njia ya bahari kutoka Efeso. 22 [mn]Alitia
nanga Kaisaria, akaenda Yerusalemu na
kulisalimu kanisa, kisha akaenda Antiokia.

## SAFARI YA TATU YA PAULO KUENEZA INJILI

*(18:23–21:16)*

23 [o]Baada ya kukaa huko kwa muda,
akaondoka na kwenda sehemu moja
hadi nyingine huko Galatia na Frigia,
akiwaimarisha wanafunzi wote.

### *Huduma Ya Apolo Huko Efeso Na Korintho*

24 [p]Basi akaja Efeso Myahudi mmoja, jina
lake Apolo, mwenyeji wa Iskanderia. Yeye
alikuwa na elimu kubwa, pia alikuwa hodari
katika Maandiko. 25 [q]Alikuwa amefundishwa
katika njia ya Bwana, naye alikuwa na bidii
katika roho, akafundisha kwa usahihi juu ya
Yesu, ingawa alijua tu ubatizo wa Yohana.
26 [r]Apolo alianza kunena kwa ujasiri

[a] **18:7** Mdo 16:14
[b] **18:8** 1Kor 1:14; Mk 5:22; Mdo 1:14
[c] **18:9** Mdo 9:10; Mt 14; 27; 1Kor 2:3
[d] **18:10** Mt 28:20
[e] **18:11** Ebr 4:12
[f] **18:12** Mdo 13:7, 8, 12; Rum 15:26; 1Kor 16:15; 2Kor 9:2; 1The 1:7
[g] **18:14** Mdo 23:29; 25:11
[h] **18:15** Mdo 23:29; 25:11, 19
[i] **18:17** 1Kor 1:1
[j] **18:18** Mdo 1:16; Rum 16:1; Hes 6:2, 5, 18
[k] **18:19** Efe 1:1; Ufu 1:11
[l] **18:21** 1Kor 4:19; Yak 4:15
[m] **18:22** Mdo 8:40; 11:19
[n] **18:22** Mdo 8:40; 21:15
[o] **18:23** Mdo 16:6; 15:32, 41
[p] **18:24** 1Kor 4:6; Tit 3:13
[q] **18:25** Rum 12:11; Mk 1:4; Mdo 19:3
[r] **18:26** Mdo 18:2

mkubwa katika sinagogi. Lakini Prisila na Akila walipomsikia, walimchukua kando na kumweleza njia ya Mungu kwa ufasaha zaidi.

[27] [a]Naye Apolo alipotaka kwenda Akaya, ndugu wa Efeso walimtia moyo, wakawaandikia wanafunzi huko ili wamkaribishe. Alipofika huko, aliwasaidia sana wale ambao, kwa neema ya Mungu, walikuwa wameamini. [28] [b]Kwa uwezo mkubwa aliwakanusha hadharani Wayahudi waliokuwa wakipinga, akionyesha kwa njia ya Maandiko kwamba Yesu ndiye Kristo.

### *Paulo Huko Efeso*

19 [c]Apolo alipokuwa huko Korintho, Paulo alisafiri sehemu za bara, akafika Efeso. Huko akawakuta wanafunzi kadhaa, [2] [d]akawauliza, “Je, mlipokea Roho Mtakatifu mlipoamini?”

Wakajibu, “Hapana, hata hatukusikia kuwa kuna Roho Mtakatifu.” [3] [e]Ndipo Paulo akawauliza, “Je, mlibatizwa kwa ubatizo gani?” Wakajibu, “Kwa ubatizo wa Yohana.”

[4] [f]Paulo akasema, “Ubatizo wa Yohana ulikuwa wa toba, aliwaambia watu wamwamini yeye atakayekuja baada yake, yaani, Yesu.” [5] [g]Waliposikia haya, wakabatizwa katika jina la Bwana Yesu. [6] [h]Paulo alipoweka mikono yake juu yao, Roho Mtakatifu akawashukia, nao wakanena kwa lugha mpya na kutabiri. [7] Walikuwa kama wanaume kumi na wawili.

[8] [i]Paulo akaingia katika sinagogi na kunena humo kwa ujasiri kwa muda wa miezi mitatu, akijadiliana na watu na kuwashawishi katika mambo ya Ufalme wa Mungu. [9] [j]Lakini baadhi yao walikaidi. Walikataa kuamini, na wakakashifu ujumbe wake mbele ya umati wa watu. Basi Paulo aliachana nao. Akawachukua wanafunzi naye, akahojiana nao kila siku katika darasa la Tirano. [10] [k]Jambo hili likaendelea kwa muda wa miaka miwili, kiasi kwamba Wayahudi na Wayunani wote walioishi huko Asia wakawa wamesikia neno la Bwana.

### *Wana Wa Skewa Wajaribu Kutoa Pepo Mchafu*

[11] [l]Mungu akafanya miujiza mingi isiyo ya kawaida kwa mkono wa Paulo, [12] [m]hivi kwamba leso au vitambaa vilivyokuwa vimegusa mwili wa Paulo viliwekwa juu ya wagonjwa, nao wakapona magonjwa yao, na pepo wachafu wakawatoka.

[13] [n]Basi baadhi ya Wayahudi wenye kutangatanga huku na huko wakitoa pepo wachafu wakajaribu kutumia jina la Bwana Yesu wale wenye pepo wakisema, “Kwa jina la Yesu, yule anayehubiriwa na Paulo, nakuamuru utoke.” [14] [o]Wana saba wa Skewa, Myahudi aliyekuwa kiongozi wa makuhani, walikuwa wanafanya hivyo. [15] [p]Lakini pepo mchafu akawajibu, “Yesu namjua na Paulo pia namjua, lakini ninyi ni nani?” [16] Kisha yule mtu aliyekuwa na pepo mchafu akawarukia, akawashambulia vikali, akawashinda nguvu wote, wakatoka ndani ya ile nyumba wakikimbia wakiwa uchi na wenye majeraha.

[17] [q]Habari hii ikajulikana kwa Wayahudi wote na Wayunani waliokaa Efeso, hofu ikawajaa wote, nalo jina la Bwana Yesu likaheshimiwa sana. [18] [r]Wengi wa wale waliokuwa wameamini wakati huu wakaja na kutubu waziwazi kuhusu matendo yao maovu. [19] Idadi kubwa ya wale waliofanya mambo ya uganga wakaleta vitabu vyao na kuviteketeza kwa moto hadharani. Walipofanya hesabu ya thamani ya vitabu

---

[a]**18:27** Mdo 18:12, 18; 1:16
[b]**18:28** Mdo 8:5; 9:12
[c]**19:1** Mdo 18:1; 18:19
[d]**19:2** Yn 20:22; Mdo 2:38
[e]**19:3** Mdo 18:25
[f]**19:4** Yn 1:7; Mdo 13:24, 25
[g]**19:5** Mdo 8:16; 2:38
[h]**19:6** Mdo 6:6; 8:17; 2:4; 10:46; Mk 16:17
[i]**19:8** Mdo 9:20; 1:3; 11:26
[j]**19:9** Mdo 14:4; 9:2
[k]**19:10** Mdo 20:31
[l]**19:11** Mdo 8:13
[m]**19:12** Mdo 5:15
[n]**19:13** Mt 12:27; Mk 9:38
[o]**19:14** Mdo 23:29; 25:11, 19
[p]**19:15** Mk 1:34; Lk 4:41
[q]**19:17** Mdo 18:19; 5:5, 11
[r]**19:18** Mt 3:6

vilivyoteketezwa ilikuwa drakma 50,000[a]
za fedha. 20 [b]Hivyo neno la Bwana likaenea
sana na kuwa na nguvu.
21 [c]Baada ya mambo haya kutukia, Paulo
akakusudia rohoni kwenda Yerusalemu
kupitia Makedonia na Akaya. Akasema,
“Baada ya kufika huko, yanipasa pia
kwenda Rumi.” 22 [d]Hivyo akatuma wasaidizi
wake wawili, Timotheo na Erasto, waende
Makedonia, wakati yeye mwenyewe alibaki
kwa muda kidogo huko Asia.

### *Ghasia Huko Efeso*

23 [e]Wakati huo huo pakatokea dhiki
kubwa kwa sababu ya Njia ile ya Bwana.
24 [f]Mtu mmoja jina lake Demetrio mfua
fedha aliyekuwa akitengeneza vinyago vya
fedha vya Artemi na kuwapatia mafundi
wake biashara kubwa, 25 [g]aliwaita pamoja
watu wengine waliofanya kazi ya ufundi
kama yake na kusema, “Enyi watu, mnajua
ya kuwa utajiri wetu unatokana na biashara
hii! 26 [h]Pia ninyi mmeona na kusikia jinsi
ambavyo si huku Efeso peke yake lakini ni
karibu Asia yote, huyu Paulo amewashawishi
na kuvuta idadi kubwa ya watu kwa kusema
kuwa miungu iliyotengenezwa na watu si
miungu. 27 Kwa hiyo kuna hatari si kwa
kazi yetu kudharauliwa tu, bali pia hata
hekalu la mungu mke Artemi, aliye mkuu,
anayeabudiwa Asia yote na ulimwengu
wote, litakuwa limepokonywa fahari yake
ya kiungu.”
28 [i]Waliposikia maneno haya,
wakaghadhibika, wakaanza kupiga kelele,
“Artemi wa Waefeso ni mkuu!” 29 [j]Mara
mji wote ukajaa ghasia. Wakawakamata
Gayo na Aristarko, watu wa Makedonia
waliokuwa wakisafiri pamoja na Paulo,
na watu wakakimbilia katika ukumbi wa
michezo kama mtu mmoja. 30 Paulo akataka
kuingia katikati ya umati huo, lakini
wanafunzi hawakumruhusu. 31 Hata baadhi
ya viongozi wa sehemu ile, waliokuwa rafiki
zake Paulo, wakatuma watu wakitamani
asiingie katika ule ukumbi.
32 [k]Ule umati ulikuwa na taharuki.
Wengine walikuwa wakipiga kelele, hawa
wakisema hili na wengine lile. Idadi
kubwa ya watu hawakujua hata ni kwa
nini walikuwa wamekusanyika huko.
33 [l]Wayahudi wakamsukumia Aleksanda
mbele na baadhi ya watu kwenye ule umati
wakampa maelekezo. Akawaashiria kwa
mkono ili watulie aweze kujitetea mbele
ya watu. 34 Lakini walipotambua kwamba
alikuwa Myahudi, wote wakapiga kelele
kwa sauti moja kwa karibu muda wa saa
mbili, wakisema, “Artemi wa Efeso ni
mkuu!”
35 [m]Baadaye karani wa mji akaunyamazisha
ule umati wa watu na kusema, “Enyi watu
wa Efeso, je, ulimwengu wote haujui ya
kuwa mji wa Efeso ndio unaotunza hekalu
la Artemi aliye mkuu na ile sanamu yake
iliyoanguka kutoka mbinguni? 36 Kwa hiyo,
kwa kuwa mambo haya hayakanushiki,
inawapasa mnyamaze na wala msifanye
lolote kwa haraka. 37 [n]Kwa kuwa mmewaleta
hawa watu hapa, ingawa hawajaiba
hekaluni wala kumkufuru huyu mungu
wetu wa kike. 38 [o]Basi, ikiwa Demetrio na
mafundi wenzake wana jambo zito dhidi
ya mtu yeyote, mahakama ziko wazi na
wasaidizi wa mwakilishi wa mtawala.
Wanaweza kufungua mashtaka. 39 Lakini
kama kuna jambo jingine lolote zaidi
mnalotaka kulileta, itabidi lisuluhishwe
katika kusanyiko halali. 40 Kama ilivyo
sasa, tuko hatarini kushtakiwa kwa kufanya
ghasia kwa sababu ya tukio la leo. Kwa

[a]19 Drakma ilikuwa ni sarafu ya fedha, thamani yake ni sawa na mshahara wa kibarua wa siku moja.
[b]**19:20** Mdo 6:7; 12:24
[c]**19:21** Mdo 21:4, 12, 15; Rum 15:25; Mdo 16:9
[d]**19:22** Mdo 13:5; 16:1; Rum 16:23; 2Tim 4:20
[e]**19:23** Mdo 9:2
[f]**19:24** Mdo 16:16, 19
[g]**19:25** Mdo 16:16, 19, 20
[h]**19:26** Mdo 16:19; Za 115:4; 1Kor 8:4
[i]**19:28** Mdo 18; 19
[j]**19:29** Rum 16:23; 1Kor 1:14; Kol 4:10; Flp 1:24; Mdo 16:9
[k]**19:32** Mdo 21:34
[l]**19:33** Mdo 12:17
[m]**19:35** Mdo 18:19
[n]**19:37** Rum 2:22
[o]**19:38** Mdo 13:7, 8, 12

kuwa hakuna sababu tutakayoweza kutoa
kuhalalisha msukosuko huu.” [41] Baada ya
kusema haya akavunja mkutano.

*Paulo Apita Makedonia Na Uyunani*

20 [a]Baada ya zile ghasia kumalizika,
Paulo aliwaita wanafunzi pamoja
akawatia moyo, akawaaga, akaanza safari
kwenda Makedonia. [2] Alipita katika sehemu
zile, akinena na watu maneno mengi ya
kuwatia moyo. Ndipo hatimaye akawasili
Uyunani, [3] [b]ambako alikaa kwa muda
wa miezi mitatu. Alipokuwa anakaribia
kuanza safari kwa njia ya bahari kwenda
Shamu, kwa sababu Wayahudi walikuwa
wamefanya shauri baya dhidi yake, aliamua
kurudi kupitia njia ya Makedonia. [4] [c]Paulo
alikuwa amefuatana na Sopatro mwana
wa Piro, Mberoya, Aristarko na Sekundo
kutoka Thesalonike na Gayo, mtu wa Derbe,
Timotheo pamoja na Tikiko na Trofimo
kutoka sehemu ya Asia. [5] [d]Hawa watu
walitutangulia wakaenda kutungojea Troa.
[6] [e]Lakini sisi tukasafiri kwa njia ya bahari
kwa siku tano kutoka Filipi baada ya siku
za Sikukuu ya Mikate Isiyotiwa Chachu,
nasi tukaungana na wengine huko Troa,
ambako tulikaa kwa siku saba.

*Eutiko Afufuliwa Huko Troa*

[7] [f]Siku ya kwanza ya juma tulikutana
pamoja kwa ajili ya kumega mkate.
Paulo akaongea na watu, naye kwa kuwa
alikuwa amekusudia kuondoka kesho
yake, aliendelea kuongea mpaka usiku wa
manane. [8] [g]Kwenye chumba cha ghorofani
walimokuwa wamekutania kulikuwa na taa
nyingi. [9] Kijana mmoja jina lake Eutiko,
alikuwa amekaa dirishani, wakati Paulo
alipokuwa akihubiri kwa muda mrefu,
alipatwa na usingizi mzito, akaanguka
kutoka ghorofa ya tatu, wakamwinua
akiwa amekufa. [10] [h]Paulo akashuka chini,
akajitupa juu yake na kumkumbatia,
akasema, “Msishtuke, uzima wake bado
umo ndani yake.” [11] [i]Kisha Paulo akapanda
tena ghorofani, akamega mkate na kula.
Baada ya kuongea mpaka mapambazuko,
akaondoka. [12] Watu wakamrudisha yule
kijana nyumbani akiwa hai nao wakafarijika
sana.

*Paulo Awaaga Wazee Wa Efeso*

[13] Tukatangulia melini tukasafiri mpaka
Aso ambako tungempakia Paulo. Alikuwa
amepanga hivyo kwa maana alitaka kufika
kwa miguu. [14] Alipotukuta huko Aso,
tulimpakia melini, tukasafiri wote mpaka
Mitilene. [15] [j]Kutoka huko tuliendelea kwa
njia ya bahari, na kesho yake tukafika
mahali panapokabili Kio. Siku iliyofuata
tukavuka kwenda Samo, na kesho yake
tukawasili Mileto. [16] [k]Paulo alikuwa
ameamua tusipitie Efeso ili asitumie muda
mwingi huko sehemu za Asia, kwa sababu
alikuwa anatamani kama ikiwezekana
kufika Yerusalemu kabla ya siku ya
Pentekoste.

[17] [l]Paulo akiwa Mileto, alituma mjumbe
kwenda Efeso kuwaita wazee wa kanisa
waje wakutane naye. [18] [m]Walipofika
akawaambia, “Ninyi wenyewe mnajua jinsi
nilivyoishi katikati yenu muda wote tangu
siku ya kwanza nilipokanyaga hapa Asia.
[19] Nilimtumikia Bwana kwa unyenyekevu
wote na kwa machozi nikivumilia taabu
na mapingamizi yaliyonipata kutokana
na hila za Wayahudi. [20] [n]Mnajua kwamba
sikusita kuhubiri jambo lolote ambalo
lingekuwa la kuwafaa ninyi, lakini
nilifundisha hadharani na nyumba kwa
nyumba. [21] [o]Nimewashuhudia Wayahudi na
Wayunani kwamba inawapasa kumgeukia

[a]**20:1** Mdo 11:26; 16:9
[b]**20:3** 2Kor 11:26; 1The 2:15-16; Mdo 16:9
[c]**20:4** Mdo 19:29; 17:19-29; 16:1; Efe 6:21; 2Tim 4:12; Mdo 21:29; 2Tim 4:20
[d]**20:5** Mdo 16:10; 16:8
[e]**20:6** Mdo 16:2; 18:8
[f]**20:7** 1Kor 16:2; Ufu 1:10
[g]**20:8** Mdo 1:13
[h]**20:10** 1Fal 17:21; 2Fal 4:34; Mt 9:23; 24
[i]**20:11** Mdo 20:7; Mt 14:19
[j]**20:15** 2Tim 4:20
[k]**20:16** Mdo 18:19; 19:21; 2:1; 1Kor 16:8
[l]**20:17** Mdo 11:30
[m]**20:18** Mdo 18:19, 21; 19:1-4
[n]**20:20** Za 40:10
[o]**20:21** Mdo 18:5; 2:38; Efe 1:15; Kol 2:5

Mungu kwa kutubu dhambi na kumwamini Bwana wetu Yesu Kristo.

[22] [a]“Nami sasa nimesukumwa na Roho, ninakwenda Yerusalemu wala sijui ni nini kitakachonipata huko. [23] [b]Ila ninachojua tu ni kwamba Roho Mtakatifu amenionya kuwa vifungo na mateso vinaningoja. [24] [c]Lakini siyahesabu maisha yangu kuwa ya thamani kwangu, kama kuyamaliza mashindano na kukamilisha ile kazi Bwana Yesu aliyonipa, yaani, kazi ya kuishuhudia Injili ya neema ya Mungu.

[25] [d]“Nami sasa najua ya kuwa hakuna hata mmoja miongoni mwenu ambaye nimemhubiria Ufalme wa Mungu katika kwenda kwangu huku na huko, atakayeniona uso tena. [26] [e]Kwa hiyo nawatangazia leo, sina hatia ya damu ya mtu awaye yote. [27] Kwa kuwa sikusita kuwatangazia mapenzi yote ya Mungu. [28] [f]Jilindeni nafsi zenu na mlilinde lile kundi lote ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi wake. Lichungeni kanisa lake Mungu alilolinunua kwa damu yake mwenyewe. [29] [g]Najua kwamba baada yangu kuondoka, mbwa mwitu wakali watakuja katikati yenu ambao hawatalihurumia kundi. [30] [h]Hata kutoka miongoni mwenu watainuka watu na kuupotosha ukweli ili wawavute wanafunzi wawafuate. [31] [i]Hivyo jilindeni! Kumbukeni kwamba kwa miaka mitatu sikuacha kamwe kuwaonya kila mmoja kwa machozi usiku na mchana.

[32] [j]“Sasa nawakabidhi kwa Mungu na kwa neno la neema yake, linaloweza kuwajenga na kuwapa ninyi urithi miongoni mwa wote ambao wametakaswa. [33] [k]Sikutamani fedha wala dhahabu wala vazi la mtu yeyote. [34] [l]Ninyi wenyewe mnajua kwamba mikono yangu hii imetumika kwa mahitaji yangu na ya wale waliokuwa pamoja nami. [35] [m]Katika kila jambo nimewaonyesha kwamba kwa njia hii ya kufanya kazi kwa bidii imetupasa kuwasaidia wadhaifu, mkikumbuka maneno ya Bwana Yesu mwenyewe jinsi alivyosema, ‘Ni heri kutoa kuliko kupokea.’ ”

[36] [n]Paulo alipomaliza kusema haya akapiga magoti pamoja nao wote akaomba. [37] [o]Wote wakalia, wakamkumbatia Paulo na kumbusu, [38] Kilichowahuzunisha zaidi ni kwa sababu ya yale maneno aliyosema kwamba kamwe hawatauona uso wake tena. Wakaenda naye mpaka kwenye meli.

*Paulo Aenda Yerusalemu*

21 [p]Tulipokwisha kujitenga nao, tukaanza safari kwa njia ya bahari moja kwa moja mpaka Kosi. Siku ya pili yake tukafika Rodo na kutoka huko tukaenda Patara. [2] [q]Hapo tukapata meli iliyokuwa inavuka kwenda Foinike tukapanda tukasafiri nayo. [3] [r]Tulipokiona kisiwa cha Kipro, tukakizunguka tukakiacha upande wetu wa kushoto, tukasafiri mpaka Shamu, tukatia nanga katika bandari ya Tiro ambapo meli yetu ilikuwa ipakue shehena yake. [4] [s]Baada ya kuwatafuta wanafunzi wa huko, tukakaa nao kwa siku saba. Wale wanafunzi wakiongozwa na Roho wakamwambia Paulo asiende Yerusalemu. [5] [t]Lakini muda wetu ulipokwisha, tukaondoka tukaendelea na safari yetu. Wale wanafunzi pamoja na wake zao na watoto wakatusindikiza hadi nje ya mji. Wote tukapiga magoti pale pwani tukaomba. [6] [u]Baada ya kuagana, tukapanda melini, nao wakarudi majumbani mwao.

[a]**20:22** Mdo 19:21
[b]**20:23** Mdo 21:4; 9:16
[c]**20:24** Mdo 21:13; 2Kor 4:1; Gal 1:1; Tit 1:3
[d]**20:25** Mt 4:23; Mdo 20:38; Rum 15:23
[e]**20:26** Mdo 18:6
[f]**20:28** 1Pet 5:2
[g]**20:29** Mt 7:15
[h]**20:30** Mdo 11:26
[i]**20:31** Mdo 19:10
[j]**20:32** Mdo 14:23; Mt 25:34; Ebr 9:15; Mdo 26:18
[k]**20:33** 1Sam 12:3; 1The 2:5
[l]**20:34** Mdo 18:3
[m]**20:35** Rum 15:1; 1Kor 9:12; 2Kor 11:9, 12; 12:13; Efe 4:28; 1The 4:11; 2The 3:8
[n]**20:36** Lk 22:41; Mdo 9:40
[o]**20:37** Lk 15:20
[p]**21:1** Mdo 16:10
[q]**21:2** Mdo 11:19
[r]**21:3** Lk 2:2
[s]**21:4** Mdo 11:26; 20:23
[t]**21:5** Mdo 20:36
[u]**21:6** Yn 1:11

7 [a]Tukaendelea na safari yetu toka Tiro
tukafika Tolemai, tukawasalimu ndugu wa
huko, tukakaa nao kwa siku moja. 8 [b]Siku
iliyofuata tukaondoka, tukafika Kaisaria.
Huko tukaenda nyumbani kwa mwinjilisti
mmoja jina lake Filipo, aliyekuwa mmoja
wa wale Saba, tukakaa kwake. 9 [c]Filipo
alikuwa na binti wanne mabikira waliokuwa
wanatoa unabii.

10 [d]Baada ya kukaa kwa siku kadhaa,
akateremka nabii mmoja kutoka Uyahudi
jina lake Agabo. 11 [e]Alipotufikia akachukua
mshipi wa Paulo akajifunga, akautumia
kufunga mikono na miguu yake mwenyewe
akasema, “Roho Mtakatifu anasema:
‘Hivi ndivyo Wayahudi wa Yerusalemu
watakavyomfunga mwenye mshipi huu na
kumkabidhi kwa watu wa Mataifa.’ ”

12 Tuliposikia maneno haya sisi na
ndugu wengine tukamsihi Paulo asiende
Yerusalemu. 13 [f]Lakini Paulo akajibu,
“Kwa nini mnalia na kunivunja moyo?
Mimi niko tayari si kufungwa tu, bali hata
kufa huko Yerusalemu kwa ajili ya jina la
Bwana Yesu.” 14 [g]Alipokuwa hashawishiki,
tukaacha kumsihi, tukasema, “Mapenzi ya
Bwana na yatendeke.”

15 [h]Baada ya haya, tukajiandaa,
tukaondoka kwenda Yerusalemu. 16 [i]Baadhi
ya wanafunzi kutoka Kaisaria wakafuatana
nasi na kutupeleka nyumbani kwa Mnasoni,
ambaye tungekaa kwake. Yeye alikuwa mtu
wa Kipro, mmoja wa wanafunzi wa zamani.

## KUKAMATWA KWA PAULO, NA SAFARI YAKE KWENDA RUMI

*(21:17–28:31)*

*Paulo Awasili Yerusalemu*

17 [j]Tulipofika Yerusalemu ndugu
wakatukaribisha kwa furaha. 18 [k]Kesho
yake Paulo pamoja na wengine wetu
tulikwenda kumwona Yakobo, na wazee
wote walikuwepo. 19 [l]Baada ya kuwasalimu,
Paulo akatoa taarifa kamili ya mambo
yote ambayo Mungu alikuwa amefanya
miongoni mwa watu wa Mataifa kupitia
huduma yake.

20 [m]Baada ya kusikia mambo haya
wakamwadhimisha Mungu. Ndipo
wakamwambia Paulo, “Ndugu, unaona
kulivyo na maelfu ya Wayahudi walioamini,
nao wote wana juhudi kwa ajili ya sheria.
21 [n]Lakini wameambiwa habari zako
kwamba unafundisha Wayahudi wote
waishio miongoni mwa watu wa Mataifa
kumkataa Mose, na kwamba unawaambia
wasiwatahiri watoto wao wala kufuata
desturi zetu. 22 Sasa tufanyeje? Bila shaka
watasikia kwamba umekuja Yerusalemu.
23 [o]Kwa hiyo fanya lile tunalokuambia.
Tunao watu wanne hapa ambao wameweka
nadhiri. 24 [p]Jiunge na watu hawa, mfanye
utaratibu wa ibada ya kujitakasa pamoja
nao, na ulipe gharama ili wanyoe nywele
zao. Kwa njia hii kila mtu atafahamu ya
kuwa mambo waliyosikia si ya kweli na
kwamba wewe unaishika sheria. 25 [q]Lakini
kuhusu wale watu wa Mataifa walioamini,
tumewaandikia uamuzi wetu: kwamba
wajitenge na vyakula vilivyotolewa sadaka
kwa sanamu, na damu, au kula nyama ya
mnyama aliyenyongwa, na wajiepushe na
uasherati.”

26 [r]Ndipo kesho yake Paulo akawachukua
wale watu na akajitakasa pamoja nao.
Akaingia ndani ya hekalu ili atoe taarifa
ya tarehe ambayo siku zao za utakaso
zingemalizika na sadaka ingetolewa kwa
ajili ya kila mmoja wao.

---

[a]**21:7** Mdo 12:20; 1:16
[b]**21:8** Efe 4:11; 2Tim 4:5; Mdo 6:5; 8:26, 40
[c]**21:9** Yoe 2:28; Mdo 2:17; Kut 15:20
[d]**21:10** Mdo 11:28
[e]**21:11** Isa 20:2, 4
[f]**21:13** Mdo 20:24
[g]**21:14** Mt 6:10; 26:42; Lk 11:2; 22:42; Rum 1:18
[h]**21:15** Mdo 19:21
[i]**21:16** Mdo 8:40
[j]**21:17** Mdo 15:4
[k]**21:18** Mdo 15; 13; 11:30
[l]**21:19** Mdo 14:27; 1:17
[m]**21:20** Gal 1:14; Flp 3:6
[n]**21:21** Mdo 15:19-21; 1Kor 7:18, 19; Mdo 6:14
[o]**21:23** Mdo 18:18
[p]**21:24** Mdo 24:18; 18:18
[q]**21:25** Mdo 15:20-29
[r]**21:26** Hes 6:13, 20; Mdo 24:18

*Paulo Akamatwa*

27 [a]Zile siku saba zilipokaribia kumalizika,
baadhi ya Wayahudi kutoka sehemu za Asia
waliokuwa wamemwona Paulo ndani ya
Hekalu, wakachochea umati wote wa watu,
nao wakamkamata. 28 [b]Wakapiga kelele
wakisema, “Waisraeli wenzetu, tusaidieni!
Huyu ndiye yule mtu anayefundisha kila
mtu na kila mahali, kinyume na watu wetu,
sheria zetu na hata Hekalu hili. Zaidi ya
hayo amewaleta Wayunani ndani ya Hekalu
na kupanajisi mahali hapa patakatifu.”
29 [c](Walikuwa wamemwona Trofimo,
mwenyeji wa Efeso, akiwa mjini pamoja
na Paulo wakadhani kuwa Paulo alikuwa
amemwingiza Hekaluni.)
30 [d]Mji wote ukataharuki, watu
wakaja wakikimbia kutoka pande zote
wakamkamata Paulo, wakamburuta kutoka
Hekaluni. Milango ya Hekalu ikafungwa.
31 Walipokuwa wakitaka kumuua, habari
zikamfikia jemadari wa jeshi la askari wa
Kirumi kwamba mji wa Yerusalemu wote
ulikuwa katika machafuko. 32 [e]Mara yule
jemadari akachukua maafisa wengine
wa jeshi pamoja na askari wakakimbilia
kwenye ile ghasia, wale watu waliokuwa
wakifanya ghasia walipomwona yule
jemadari na askari wakija, wakaacha
kumpiga Paulo.
33 [f]Yule jemadari akaja, akamkamata
Paulo akaamuru afungwe kwa minyororo
miwili. Akauliza yeye ni nani, na alikuwa
amefanya nini. 34 [g]Baadhi ya watu katika
ule umati wakapiga kelele, hawa wakisema
hili na wengine lile. Yule jemadari alipoona
kuwa hawezi kupata hakika ya habari
kwa sababu ya zile kelele, akaamuru
Paulo apelekwe katika ngome ya jeshi.
35 [h]Paulo alipofika penye ngazi, ilibidi askari
wambebe juu juu kwa sababu fujo za ule
umati wa watu zilikuwa kubwa. 36 [i]Umati
wa watu ulikuwa ukifuata ukiendelea
kupiga kelele ukisema, “Mwondoe huyu!”

*Paulo Anajitetea*

37 [j]Mara tu Paulo alipokaribia kuingizwa
kwenye ngome ya jeshi, akamwambia yule
jemadari, “Je, naweza kukuambia jambo
moja?”
Yule jemadari akamjibu, “Je, unajua
Kiyunani? 38 [k]Je, wewe si yule Mmisri
ambaye siku hizi za karibuni alianzisha uasi
akaongoza kundi la magaidi 4,000 wenye
silaha jangwani?”
39 [l]Paulo akajibu, “Mimi ni Myahudi,
mzaliwa wa Tarso, huko Kilikia, raiya
wa mji maarufu. Tafadhali niruhusu
nizungumze na hawa watu.”
40 [m]Akiisha kupata ruhusa ya yule
jemadari, Paulo akasimama penye ngazi
akawapungia watu mkono ili wanyamaze.
Wote waliponyamaza kimya, Paulo
akazungumza nao kwa lugha ya Kiebrania,
akasema:

*Ushuhuda Wa Paulo Kwa Wayahudi Wa Yerusalemu*

22 [n]“Ndugu zangu na baba zangu,
sikilizeni utetezi wangu.”
2 [o]Waliposikia akisema kwa lugha ya
Kiebrania, wakanyamaza kimya kabisa.
Ndipo Paulo akasema, 3 [p]“Mimi ni
Myahudi, niliyezaliwa Tarso huko Kilikia,
lakini nimelelewa katika mji huu. Miguuni
mwa Gamalieli, nilifundishwa kikamilifu
katika sheria ya baba zetu, na nikawa
mwenye juhudi kwa ajili ya Mungu kama
kila mmoja wenu alivyo leo. 4 [q]Niliwatesa
watu wa Njia hii hadi kufa, nikiwakamata
waume kwa wake na kuwatupa gerezani,

---

[a]**21:27** Yer 26:8; 1The 2:16
[b]**21:28** Mt 24; 15; Mdo 6:13
[c]**21:29** Mdo 20:4; 18:19
[d]**21:30** Mdo 26:26; 16:19
[e]**21:32** Mdo 23:27
[f]**21:33** Mdo 12:6; Efe 6:20; 2Tim 2:9
[g]**21:34** Mdo 19:32; 22:24
[h]**21:35** Mdo 21:40
[i]**21:36** Lk 23:18; Yn 19:15
[j]**21:37** Mdo 21:34
[k]**21:38** Mt 24:26; Mdo 5:36
[l]**21:39** Mdo 9:11; 23:3
[m]**21:40** Mdo 12:17; Yn 5:2
[n]**22:1** Mdo 7:2
[o]**22:2** Mdo 21:40
[p]**22:3** Mdo 9:11; Lk 10:39; Mdo 5:34; 26:5; 21:20
[q]**22:4** Mdo 8:3

5 [a]kama kuhani mkuu na baraza zima la wazee wanavyoweza kushuhudia kunihusu. Hata nilipokea barua kutoka kwao kwenda kwa ndugu wale wa Dameski, nami nikaenda huko ili kuwaleta watu hawa Yerusalemu kama wafungwa ili waadhibiwe.

*Paulo Aeleza Juu Ya Kuokoka Kwake*

**(Matendo 9:1-19; 26:12-18)**

6 [b]“Nilipokuwa njiani kuelekea Dameski, yapata saa sita mchana, ghafula nuru kubwa kutoka mbinguni ikanimulika kotekote. 7 Nikaanguka chini, nikasikia sauti ikiniambia, ‘Sauli, Sauli! Mbona unanitesa?’

8 [c]“Nikajibu, ‘Wewe ni nani Bwana?’

“Naye akaniambia, ‘Mimi ni Yesu wa Nazareti unayemtesa.’ 9 [d]Basi wale watu waliokuwa pamoja nami waliiona ile nuru, lakini hawakuisikia sauti ya yule aliyekuwa akisema nami.

10 [e]“Nikauliza, ‘Nifanye nini Bwana?’

“Naye Bwana akaniambia, ‘Inuka uingie Dameski, huko utaambiwa yote yakupasayo kufanya.’ 11 [f]Kwa kuwa nilikuwa siwezi kuona kwa ajili ya mng’ao wa ile nuru, wenzangu wakanishika mkono wakaniongoza kuingia Dameski.

12 [g]“Mtu mmoja mcha Mungu, jina lake Anania, alikuja kuniona. Alizishika sana sheria zetu, na aliheshimiwa sana na Wayahudi waliokuwa wakiishi huko Dameski. 13 Akasimama karibu nami, akasema, ‘Ndugu Sauli, pata kuona tena!’ Saa ile ile nikapata kuona tena, nami nikaweza kumwona.

14 [h]“Akasema, ‘Mungu wa baba zetu amekuchagua wewe ili ujue mapenzi yake, umwone yeye Aliye Mwenye Haki na upate kusikia maneno kutoka kinywani mwake. 15 [i]Kwa kuwa utakuwa shahidi wake kwa watu kuhusu kile ulichokiona na kukisikia. 16 [j]Sasa basi, mbona unakawia? Inuka, ukabatizwe na dhambi zako zikasafishwe, ukiliita Jina lake.’

*Paulo Atumwa Kwa Watu Wa Mataifa*

17 [k]“Baada ya kurudi Yerusalemu, nilipokuwa ninaomba Hekaluni, nilipitiwa na usingizi wa ghafula 18 [l]nikamwona Bwana akiniambia, ‘Harakisha utoke Yerusalemu upesi, maana hawataukubali ushuhuda wako kunihusu mimi.’

19 [m]“Nami nikasema, ‘Bwana, wao wenyewe wanajua jinsi nilivyokwenda kwenye kila sinagogi ili kuwatupa gerezani na kuwapiga wale waliokuamini. 20 [n]Wakati damu ya shahidi wako Stefano ilipomwagwa, mimi mwenyewe nilikuwa nimesimama kando, nikikubaliana na kitendo hicho na kutunza mavazi ya wale waliomuua.’

21 [o]“Ndipo Bwana akaniambia, ‘Nenda, kwa maana nitakutuma mbali, kwa watu wa Mataifa.’ ”

*Paulo Na Jemadari Wa Kirumi*

22 [p]Ule umati wa watu wakamsikiliza Paulo mpaka aliposema neno hilo, ndipo wakapaza sauti zao na kupiga kelele wakisema, “Mwondoeni duniani, hafai kuishi!”

23 [q]Walipokuwa wakipiga kelele na kutoa mavazi yao huku wakirusha mavumbi juu hewani, 24 [r]yule jemadari akaamuru Paulo aingizwe kwenye ngome. Akaelekeza kwamba achapwe viboko na aulizwe ili kujua kwa nini watu walikuwa wanampigia kelele namna hiyo. 25 [s]Lakini walipokwisha kumfunga kwa kamba za ngozi ili wamchape viboko, Paulo akamwambia kiongozi wa

---

[a]**22:5** Lk 22:66; Rum 7:1; Mdo 9:2
[b]**22:6** Mdo 9:3
[c]**22:8** Mk 1:24
[d]**22:9** Mdo 26:13; 9:7
[e]**22:10** Mdo 16:30
[f]**22:11** Mdo 9:8
[g]**22:12** Mdo 9:17; 19:22
[h]**22:14** Mdo 3:13; 1Kor 9:1; 15:8; Mdo 7:52
[i]**22:15** Mdo 23:11; 26:16
[j]**22:16** Mdo 2:38; Za 51:2; Rum 10:13
[k]**22:17** Mdo 9:26; 10:10
[l]**22:18** Mdo 22:14; Mt 10:14
[m]**22:19** Mdo 8:3; Mt 10:17
[n]**22:20** Mdo 7:57-60; 8:1
[o]**22:21** Mdo 9:15; 13:46
[p]**22:22** Mdo 21:36
[q]**22:23** Mdo 7:58; 2Sam 16:13
[r]**22:24** Mdo 21:34
[s]**22:25** Mdo 16:37

askari aliyekuwa amesimama pale karibu naye, "Je, ni halali kwenu kwa mujibu wa sheria kumchapa mtu ambaye ni raiya wa Rumi hata kabla hajapatikana na hatia?"

26 Yule kiongozi aliposikia maneno haya, alimwendea yule jemadari na kumwambia, "Unataka kufanya nini? Kwa maana huyu mtu ni raiya wa Rumi."

27 Yule jemadari akaja akamuuliza Paulo, "Niambie, wewe ni raiya wa Rumi?"

Paulo akajibu, "Naam, hakika ndiyo."

28 Ndipo yule jemadari akasema, "Mimi ilinigharimu kiasi kikubwa cha fedha kupata uraia wangu."

Paulo akasema "Lakini mimi ni raiya wa Rumi kwa kuzaliwa."

29 [a]Mara wale waliokuwa wanataka kumhoji wakajiondoa haraka, naye yule jemadari akaingiwa na hofu alipotambua ya kuwa amemfunga Paulo, ambaye ni raia wa Rumi, kwa minyororo.

*Paulo Apelekwa Mbele Ya Baraza*

30 [b]Kesho yake, kwa kuwa yule jemadari alitaka kujua hakika kwa nini Paulo alikuwa anashutumiwa na Wayahudi, alimfungua, na akawaagiza viongozi wa makuhani na baraza lote likutane. Kisha akamleta Paulo, akamsimamisha mbele yao.

23 [c]Paulo akawakazia macho wale wajumbe wa baraza, akasema, "Ndugu zangu, nimetimiza wajibu wangu kwa Mungu kwa dhamiri safi kabisa hadi leo."
2 [d]Kwa ajili ya jambo hili kuhani mkuu Anania akaamuru wale waliokuwa karibu na Paulo wampige kofi kinywani. 3 [e]Ndipo Paulo akamwambia, "Mungu atakupiga wewe, ewe ukuta uliopakwa chokaa! Wewe umeketi hapo ili kunihukumu kwa mujibu wa sheria, lakini wewe mwenyewe unakiuka sheria kwa kuamuru kwamba nipigwe kinyume cha sheria!"

4 Wale watu waliokuwa wamesimama karibu na Paulo wakamwambia, "Je, wewe wathubutu kumtukana kuhani mkuu wa Mungu?"

5 [f]Paulo akajibu, "Ndugu zangu, sikujua kwamba yeye alikuwa kuhani mkuu. Kwa maana imeandikwa, 'Usimnenee mabaya kiongozi wa watu wako.' "

6 [g]Paulo alipotambua ya kuwa baadhi yao walikuwa Masadukayo na wengine ni Mafarisayo, akapaza sauti kwenye baraza, "Ndugu zangu, mimi ni Farisayo, mwana Farisayo. Hapa nimeshtakiwa kuhusu tumaini langu katika ufufuo wa wafu."
7 Aliposema haya, farakano likaanza kati ya Mafarisayo na Masadukayo na baraza lote
likagawanyika. 8 [h](Kwa maana Masadukayo wanasema kwamba hakuna ufufuo, wala hakuna malaika au roho, lakini Mafarisayo wanaamini haya yote.)

9 [i]Kukawa na ghasia kubwa, nao baadhi ya walimu wa sheria ambao ni Mafarisayo, wakasimama wakapinga kwa nguvu wakisema, "Hatuoni kosa lolote la mtu huyu! Huenda ikawa roho au malaika
amezungumza naye" 10 [j]Ugomvi ukawa mkubwa kiasi kwamba yule jemadari akahofu kuwa wangemrarua Paulo vipande vipande, akaamuru vikosi vya askari vishuke na kumwondoa Paulo katikati yao kwa nguvu na kumleta ndani ya ngome ya jeshi.

11 [k]Usiku uliofuata, Bwana akasimama karibu naye akamwambia, "Jipe moyo! Kama vile ulivyonishuhudia hapa Yerusalemu, hivyo imekupasa kunishuhudia huko Rumi pia."

*Hila Za Kumuua Paulo*

12 [l]Kulipopambazuka Wayahudi wakafanya shauri pamoja na kujifunga kwa kiapo kwamba hawatakula wala

[a]**22:29** Mdo 16:38
[b]**22:30** Mdo 23:28; 21:33; Mt 5:22
[c]**23:1** Mdo 22:30; 22:5; 1Tim 3:9; Ebr 10:22
[d]**23:2** Mdo 24:1; Yn 14:22
[e]**23:3** Mt 23:27; Law 19:15; Yn 7:31
[f]**23:5** Kut 22:28
[g]**23:6** Mdo 22:5; 26:5; 21:15, 21; 26:8; Flp 3:5
[h]**23:8** Mt 22:23; Mk 2:16; Lk 23:4; Mdo 22:7, 17, 18
[i]**23:9** Mdo 25:25; 5:39; Mk 2:16; Mdo 23:29; Yer 26:16; Lk 23:4; Mdo 26:31; 28:18; 22:7; 18:18
[j]**23:10** Mdo 21:34
[k]**23:11** Mdo 18:9; 19:21; 28:23
[l]**23:12** Mdo 20:3; 25:3; 25:3

kunywa mpaka wawe wamemuua Paulo.
13 Waliofanya mpango huo walikuwa
zaidi ya watu arobaini. 14 [a]Wakawaendea
viongozi wa makuhani na wazee na
kusema, "Tumejifunga pamoja kwa kiapo
kwamba hatutakula wala kunywa mpaka
tuwe tumemuua Paulo. 15 [b]Hivyo basi, wewe
pamoja na baraza, inawapasa mkamjulishe
jemadari ili amteremshe Paulo kwenu,
mjifanye kama mnataka kufanya uchunguzi
wa kina zaidi wa shauri lake. Nasi tuko
tayari kumuua kabla hajafika hapa."
16 Lakini mtoto wa dada yake Paulo
aliposikia juu ya shauri hilo baya,
alikwenda kule kwenye ngome ya askari
na kumweleza Paulo.
17 Ndipo Paulo akamwita mmoja wa
viongozi wa askari, akamwambia, "Mpeleke
huyu kijana kwa jemadari, analo jambo
la kumweleza." 18 [c]Hivyo yule kiongozi
wa askari akampeleka yule kijana kwa
jemadari, akamwambia, "Paulo yule
mfungwa aliniita na kuniomba nimlete
huyu kijana kwako, kwa sababu ana neno
la kukueleza."
19 Yule jemadari akamshika yule kijana
mkono, akampeleka kando na kumuuliza,
"Unataka kuniambia nini?"
20 [d]Yule kijana akasema, "Wayahudi
wamekubaliana wakuombe umpeleke Paulo
kwenye baraza lao kesho kwa kisingizio
kwamba wanataka kufanya uchunguzi wa
kina wa shauri lake. 21 Lakini usishawishiwe
nao kwa maana zaidi ya watu arobaini
wanamvizia. Wamejifunga kwa kiapo
kwamba hawatakula wala kunywa mpaka
wawe wamemuua Paulo. Sasa wako tayari,
wanangoja idhini yako kwa ajili ya ombi
lao."
22 Yule jemadari akamruhusu yule
kijana aende na akamwonya, akisema,
"Usimwambie mtu yeyote kwamba
umenieleza habari hizi."

[a]**23:14** Mdo 23:1; 14:15
[b]**23:15** Mdo 22:30
[c]**23:18** Efe 3:1
[d]**23:20** Mdo 23:13

*Paulo Ahamishiwa Kaisaria*

23 [e]Kisha yule jemadari akawaita viongozi
wake wawili wa askari akawaambia,
"Jiandaeni kuondoka saa tatu usiku
huu kuelekea Kaisaria pamoja na askari
200, wapanda farasi sabini na watu 200
wenye mikuki. 24 [f]Pia tayarisheni na farasi
watakaotumiwa na Paulo, mkampeleke
salama kwa mtawala Feliksi."
25 Kisha akaandika barua kwa Feliksi
kama ifuatavyo:

26 [g]Klaudio Lisia,

Kwa Mtawala, Mtukufu Feliksi:

Salamu.

27 [h]Mtu huyu alikamatwa na
Wayahudi wakakaribia kumuua,
lakini nikaja na vikosi vyangu vya
askari nikamwokoa, kwa kuwa nilipata
habari kwamba yeye ni raiya wa Rumi.
28 [i]Nilitaka kujua kwa nini walikuwa
wanamshutumu, hivyo nikamleta
mbele ya baraza lao. 29 [j]Ndipo
nikaona kuwa alikuwa anashutumiwa
kwa mambo yanayohusu sheria
yao, lakini hakuwa ameshtakiwa
kwa jambo lolote linalostahili kifo
au kifungo. 30 [k]Nilipoarifiwa kuwa
kulikuwa na shauri baya dhidi ya mtu
huyu, nilimtuma kwako mara moja.
Niliwaagiza washtaki wake pia waeleze
mashtaka yao dhidi yake mbele yako.

31 Hivyo askari, kwa kufuata maelekezo
waliyopewa, wakamchukua Paulo wakati
wa usiku na kumleta mpaka Antipatri.
32 [l]Kesho yake wakawaacha wale wapanda
farasi waendelee na safari wakiwa na Paulo,
wao wakarudi kwenye ngome ya askari.
33 [m]Askari walipofika Kaisaria, walimpa
mtawala ile barua, na kumkabidhi Paulo

[e]**23:23** Mdo 8:40
[f]**23:24** Mdo 24:1-3, 10; 25; 14
[g]**23:26** Mdo 25:14; 15:23
[h]**23:27** Mdo 21:32; 21:33; 22:25-29
[i]**23:28** Mdo 22:30
[j]**23:29** Mdo 18:15; 25:19; 26:31
[k]**23:30** Mdo 20:3; 24:19; 25:16
[l]**23:32** Mdo 21:34
[m]**23:33** Mdo 8:40

kwake. 34 [a]Mtawala alipokwisha kuisoma
ile barua alimuuliza Paulo alikuwa mtu
wa jimbo gani. Alipojua kuwa anatoka
Kilikia, 35 [b]alisema, “Nitasikiliza shauri lako
washtaki wako watakapofika hapa.” Kisha
akaamuru Paulo awekwe chini ya ulinzi
kwenye jumba la kifalme la Herode.

*Mbele Ya Feliksi Huko Kaisaria*

24 [c]Baada ya siku tano, kuhani mkuu
Anania akashuka akiwa amefuatana na
baadhi ya wazee pamoja na mwanasheria
mmoja aitwaye Tertulo, nao wakaleta
mashtaka yao dhidi ya Paulo mbele
ya mtawala. 2 [d]Paulo alipoitwa aingie
ndani, Tertulo akaanza kutoa mashtaka
akisema, “Mtukufu Feliksi, kwa muda
mrefu tumefurahia amani na matengenezo
mengi mazuri yamefanywa kwa ajili ya
watu hawa kwa sababu ya upeo wako wa
kuona mambo ya mbele. 3 [e]Wakati wote na
kila mahali, kwa namna yoyote, mtukufu
sana Feliksi, tumeyapokea mambo haya
yote kwa shukrani nyingi. 4 Lakini nisije
nikakuchosha zaidi, ningekuomba kwa
hisani yako utusikilize kwa kifupi.

5 [f]“Tumemwona mtu huyu kuwa ni
msumbufu, anayechochea ghasia miongoni
mwa Wayahudi duniani pote. Yeye ndiye
kiongozi wa dhehebu la Wanazarayo, 6 [g]na
hata amejaribu kulinajisi Hekalu, hivyo
tukamkamata; [tukataka kumhukumu
kufuatana na sheria zetu. 7 Lakini jemadari
Lisia alitujia na nguvu nyingi, akamwondoa
mikononi mwetu, 8 akiwaamuru
washtaki wake waje mbele yako: ili]
kwa kumchunguza wewe mwenyewe
unaweza kujua kutoka kwake mambo yote
tunayomshtaki kwayo.”

9 [h]Pia wale Wayahudi wakaunga mkono
wakithibitisha kuwa mashtaka yote haya
ni kweli.

*Paulo Ajitetea Mbele Ya Feliksi*

10 [i]Mtawala Feliksi alipompungia Paulo
mkono ili ajitetee, yeye akajibu, “Najua
kwamba wewe umekuwa hakimu katika
taifa hili kwa miaka mingi, hivyo natoa
utetezi wangu kwa furaha. 11 [j]Unaweza
kuhakikisha kwa urahisi kuwa hazijapita
zaidi ya siku kumi na mbili tangu
nilipopanda kwenda Yerusalemu kuabudu.
12 [k]Hawa wanaonishtaki hawakunikuta
nikibishana na mtu yeyote Hekaluni au
kuchochea umati wa watu katika sinagogi
au mahali pengine popote mjini. 13 [l]Wala
hawawezi kabisa kukuthibitishia mashtaka
haya wanayonishtaki kwayo. 14 [m]Lakini,
ninakubali kwamba mimi namwabudu
Mungu wa baba zetu, mfuasi wa Njia, ile
ambayo wao wanaiita dhehebu. Ninaamini
kila kitu kinachokubaliana na Sheria na
kile kilichoandikwa katika Manabii,
15 [n]nami ninalo tumaini kwa Mungu,
ambalo hata wao wenyewe wanalikubali
kwamba kutakuwa na ufufuo wa wafu, kwa
wenye haki na wasio na haki. 16 [o]Kwa hiyo
ninajitahidi siku zote kuwa na dhamiri safi
mbele za Mungu na mbele za wanadamu.

17 [p]“Basi, baada ya kutokuwepo kwa
miaka mingi nilikuja Yerusalemu ili
kuwaletea watu wangu msaada kwa ajili
ya maskini na kutoa dhabihu. 18 [q]Nilikuwa
nimeshatakaswa kwa taratibu za kiibada
waliponikuta Hekaluni nikifanya mambo
haya. Hapakuwa na umati wa watu, pamoja
nami wala aliyehusika kwenye fujo yoyote.
19 [r]Lakini kulikuwa na baadhi ya Wayahudi
kutoka Asia, ambao wangelazimika wawepo

[a]**23:34** Mdo 6:9; 21:39
[b]**23:35** Mdo 24:19; 25:16; 24:27
[c]**24:1** Mdo 23:2; 23:30-35; 23:24
[d]**24:2** Lk 1:3; Mdo 23:26
[e]**24:3** Lk 1:3; Mdo 23:26; 26:25
[f]**24:5** Mdo 16:20; 17:6; 21:28; Mk 1:24; Mdo 28:22
[g]**24:6** Mdo 21:28
[h]**24:9** 1The 2:16
[i]**24:10** Mdo 23:24
[j]**24:11** Mdo 21:27
[k]**24:12** Mdo 25:8; 28:17
[l]**24:13** Mdo 25:7
[m]**24:14** Mdo 3:13; 9:2; 26:6, 22; 28:23
[n]**24:15** Mdo 23:6; 28:20; Dan 12:12; Mt 25:46
[o]**24:16** Mdo 23:1
[p]**24:17** Mdo 11:29, 30; Rum 15:25-28, 31; 1Kor 16:1-4, 15; 2Kor 8:1-4; Gal 2:10
[q]**24:18** Mdo 21:26
[r]**24:19** Mdo 23:30

hapa mbele yako ili watoe mashtaka kama
wanalo jambo lolote dhidi yangu. 20 Au,
watu hawa walioko hapa waseme ni uhalifu
gani walioniona nao waliponisimamisha
mbele ya baraza, 21 [a]isipokuwa ni kuhusu
jambo hili moja nililopiga kelele mbele yao
kwamba, 'Mimi nashtakiwa mbele yenu leo
kwa sababu ya ufufuo wa wafu.' "
22 [b]Basi Feliksi ambaye alikuwa anafahamu
vizuri habari za Njia ile, akaahirisha shauri
lile kwa maelezo yake akisema, "Wakati
jemadari Lisia atakapoteremka huku,
nitaamua shauri lako." 23 [c]Ndipo akaamuru
kiongozi wa askari amweke chini ya ulinzi
lakini ampe uhuru na kuwaruhusu rafiki
zake wamhudumie.
24 [d]Baada ya siku kadhaa, Feliksi alikuja
pamoja na Drusila mkewe, ambaye alikuwa
Myahudi. Alituma aitiwe Paulo, naye
akamsikiliza alipokuwa akinena juu ya
imani katika Kristo Yesu. 25 [e]Naye Paulo
alipokuwa akinena juu ya haki, kuwa
na kiasi na juu ya hukumu ijayo, Feliksi
aliingiwa na hofu na kusema, "Hiyo yatosha
sasa! Waweza kuondoka. Nitakapokuwa
na wasaa nitakuita." 26 Wakati huo Feliksi
alitazamia kwamba Paulo angempa rushwa.
Hivyo akawa anamwita mara kwa mara na
kuzungumza naye.
27 [f]Baada ya miaka miwili kupita, Porkio
Festo akaingia kwenye utawala mahali pa
Feliksi, lakini kwa kuwa Feliksi alitaka
kuwapendeza Wayahudi, akamwacha Paulo
gerezani.

### *Paulo Mbele Ya Festo*

25 [g]Siku tatu baada ya Festo kuwasili
Kaisaria kuchukua wajibu wake mpya,
alipanda kwenda Yerusalemu, 2 [h]ambako
viongozi wa makuhani na viongozi wa
Wayahudi walikuja mbele yake na kuleta
mashtaka yao dhidi ya Paulo. 3 [i]Wakamsihi
sana Festo, kama upendeleo kwao, aamuru
Paulo ahamishiwe Yerusalemu, kwa kuwa
walikuwa wanaandaa kumvizia ili wamuue
akiwa njiani. 4 [j]Festo akawajibu, "Paulo
amezuiliwa huko Kaisaria, nami mwenyewe
ninakwenda huko hivi karibuni. 5 Baadhi
ya viongozi wenu wafuatane nami na kutoa
mashtaka dhidi ya mtu huyo huko, kama
amekosa jambo lolote."
6 [k]Baada ya Festo kukaa miongoni mwao
kwa karibu siku nane au kumi, akashuka
kwenda Kaisaria na siku iliyofuata akaitisha
mahakama, akaketi penye kiti chake cha
hukumu, akaamuru Paulo aletwe mbele
yake. 7 [l]Paulo alipotokea, wale Wayahudi
waliokuwa wameteremka toka Yerusalemu
wakasimama wakiwa wamemzunguka,
wakileta mashtaka mengi mazito dhidi
yake ambayo hawakuweza kuyathibitisha.
8 [m]Ndipo Paulo akajitetea, akasema,
"Mimi sikufanya jambo lolote kinyume cha
sheria ya Wayahudi au dhidi ya Hekalu au
kinyume cha Kaisari."
9 [n]Festo, akitaka kuwapendeza Wayahudi,
akamuuliza Paulo, "Je, ungependa kwenda
Yerusalemu na kukabili mashtaka mbele
yangu huko?"
10 [o]Paulo akasema, "Mimi sasa nimesimama
mbele ya mahakama ya Kaisari, ambako
ndiko ninakostahili kushtakiwa. Kama vile
wewe mwenyewe ujuavyo vyema kabisa
sijawatendea Wayahudi kosa lolote. 11 [p]Basi
kama mimi nina hatia ya kutenda kosa
lolote linalostahili kifo, sikatai kufa. Lakini
kama mashtaka yaliyoletwa dhidi yangu na
hawa Wayahudi si kweli, hakuna yeyote
aliye na haki ya kunikabidhi mikononi
mwao. Naomba rufaa kwa Kaisari!"
12 Baada ya Festo kufanya shauri pamoja
na baraza lake, akatangaza, "Wewe

---

[a]**24:21** Mdo 23:6
[b]**24:22** Mdo 9:2; 24:7
[c]**24:23** Mdo 23:35; 28:16; 23:16; 27:3
[d]**24:24** Mdo 20:21
[e]**24:25** Gal 5:23; 1Pet 4:7; Mdo 10:42
[f]**24:27** Mdo 25:1, 4, 9, 14; 12:3; 25:9; 23:35; 25:14
[g]**25:1** Mdo 8:40
[h]**25:2** Mdo 24:1
[i]**25:3** Mdo 23:12, 15; 20:3
[j]**25:4** Mdo 24:23
[k]**25:6** Mdo 25:17
[l]**25:7** Mk 15:3; Lk 23:2, 10; Mdo 24:13
[m]**25:8** Mdo 6:13; 28:17
[n]**25:9** Mdo 12:3; 24:27
[o]**25:10** Mdo 25:8
[p]**25:11** Mdo 26:32; 28:19

umeomba rufaa kwa Kaisari, nako kwa
Kaisari utakwenda!”

### *Festo Aomba Ushauri Kwa Agripa*

13 [a]Baada ya siku kadhaa Mfalme Agripa
na Bernike wakapanda kuja Kaisaria
kumsalimu Festo. 14 Kwa kuwa walikuwa
wakae huko Kaisaria kwa siku nyingi,
Festo alijadili shauri la Paulo na mfalme,
akisema, “Kuna mtu mmoja hapa ambaye
Feliksi alimwacha gerezani. 15 Nilipokuwa
huko Yerusalemu, viongozi wa makuhani
na wazee wa Wayahudi walinijulisha habari
zake na wakaomba hukumu dhidi yake.

16 “Lakini mimi nikawaambia kwamba
si desturi ya Kirumi kumtoa mtu yeyote
auawe kabla mshtakiwa kuonana uso kwa
uso na washtaki wake, naye awe amepewa
nafasi ya kujitetea kuhusu mashtaka
anayoshutumiwa. 17 Hivyo walipokutana
hapa, sikukawia, kesho yake niliitisha baraza,
nikaketi penye kiti changu cha hukumu,
nikaagiza huyo mtu aletwe. 18 Washtaki
wake waliposimama, hawakushtaki kwa
uhalifu wowote niliokuwa ninatarajia.
19 Badala yake walikuwa na vipengele
fulani vya kutokukubaliana naye kuhusu
dini yao na juu ya mtu mmoja aitwaye
Yesu, ambaye alikufa, lakini yeye Paulo
alidai kwamba yu hai. 20 Kwa kuwa sikujua
jinsi ya kupeleleza jambo hili, nilimuuliza
kama angependa kwenda Yerusalemu na
kuhojiwa huko kuhusu mashtaka haya.
21 Lakini Paulo alipoomba afadhiliwe ili
rufaa yake isikilizwe na Mfalme Agusto,
nilimwamuru alindwe mpaka nitakapoweza
kumpeleka kwa Kaisari.”

22 Ndipo Agripa akamwambia Festo,
“Ningependa kumsikiliza mtu huyo mimi
mwenyewe.”

Yeye akajibu, “Kesho utamsikia.”

### *Paulo Aletwa Mbele Ya Agripa*

23 Siku iliyofuata Agripa na Bernike
walifika kwa fahari kubwa wakaingia
katika ukumbi wa mahakama, pamoja na
majemadari wa jeshi na watu mashuhuri
wa mji. Ndipo kwa amri ya Festo, Paulo
akaletwa ndani. 24 Festo akasema, “Mfalme
Agripa, nanyi nyote mlio hapa pamoja nasi,
mnamwona mtu huyu! Jumuiya yote ya
Kiyahudi wamenilalamikia kuhusu mtu
huyu huko Yerusalemu na hapa Kaisaria,
wakipiga kelele kwamba haimpasi kuendelea
kuishi. 25 Sikuona kwamba ametenda jambo
lolote linalostahili kifo, ila kwa kuwa
alikuwa ameomba rufaa yake kwa mfalme,
niliamua kumpeleka Rumi. 26 Lakini mimi
sina kitu maalum cha kumwandikia Bwana
Mtukufu kumhusu mtu huyu. Kwa hiyo
nimemleta mbele yenu ninyi nyote, hasa
mbele yako, Mfalme Agripa, ili kutokana na
matokeo ya uchunguzi huu, niweze kupata
kitu cha kuandika. 27 Kwa kuwa naona
hakuna sababu ya kumpeleka mfungwa
bila kuainisha mashtaka dhidi yake.”

### *Paulo Ajitetea Mbele Ya Agripa*

26 [b]Ndipo Agripa akamwambia Paulo,
“Unayo ruhusa kujitetea.”

Hivyo Paulo akawaashiria kwa mkono
wake, akaanza kujitetea, akasema:
2 [c]“Mfalme Agripa, najiona kuwa na heri
kusimama mbele yako leo ninapojitetea
kuhusu mashtaka yote ya Wayahudi, 3 [d]hasa
kwa sababu unajua vyema desturi zote za
Kiyahudi na ya kuwa wewe unajua kwa
undani mila na masuala ya mabishano. Kwa
hiyo, nakusihi unisikilize kwa uvumilivu.

4 [e]“Wayahudi wote wanajua jinsi
nilivyoishi tangu nilipokuwa mtoto,
kuanzia mwanzo wa maisha yangu katika
nchi yangu na pia huko Yerusalemu.
5 [f]Wao wamefahamu kwa muda mrefu na
wanaweza kushuhudia kama wakipenda,
ya kwamba kutokana na misimamo mikali
sana ya dhehebu letu kwenye dini yetu,
niliishi nikiwa Farisayo. 6 [g]Nami sasa ni
kwa sababu ya tumaini langu katika kile
ambacho Mungu aliwaahidi baba zetu,

---

[a]**25:13** Mdo 8:40

[b]**26:1** Mdo 9:15; 25:22

[c]**26:2** Za 119:46; Mdo 24:1, 5; 25:2; 7:11

[d]**26:3** Mdo 6:14; 25:19

[e]**26:4** Gal 1:13, 14; Flp 3:5

[f]**26:5** Mdo 22:3; 24:15; 28:20; 13:32; Rum 15:8

[g]**26:6** Mdo 23:6; 24:15; 28:20; 13:32; Rum 15:8

ninashtakiwa leo. [7] [a]Hii ndiyo ahadi ambayo
makabila yetu kumi na mawili yanatarajia
kuiona ikitimizwa wanapomtumikia
Mungu kwa bidii usiku na mchana. Ee
mfalme, ninashtakiwa na Wayahudi kwa
ajili ya tumaini hili. [8] [b]Kwa nini yeyote
miongoni mwenu afikiri kwamba ni jambo
lisilosadikika Mungu kufufua wafu?

[9] [c]“Mimi pia nilikuwa nimeshawishika
kwamba imenipasa kufanya yote yale
yaliyowezekana kupinga Jina la Yesu wa
Nazareti. [10] [d]Nami hayo ndiyo niliyoyafanya
huko Yerusalemu. Kwa mamlaka ya
viongozi wa makuhani, niliwatia wengi
wa watakatifu gerezani na walipokuwa
wakiuawa, nilipiga kura yangu kuunga
mkono. [11] [e]Mara nyingi nilikwenda kutoka
sinagogi moja hadi ingine nikiamuru
waadhibiwe, nami nilijaribu kuwalazimisha
wakufuru. Katika shauku yangu dhidi yao,
hata nilikwenda miji ya kigeni ili kuwatesa.

### *Paulo Aeleza Kuhusu Kuokoka Kwake*

**(Matendo 9:1-19; 22:6-16)**

[12] “Siku moja nilipokuwa katika mojawapo
ya safari hizi nikiwa ninakwenda Dameski,
nilikuwa na mamlaka na agizo kutoka kwa
kiongozi wa makuhani. [13] Ilikuwa yapata
adhuhuri, ee mfalme, nilipokuwa njiani,
niliona nuru kutoka mbinguni kali kuliko
jua, iking’aa kunizunguka pande zote mimi
na wale niliokuwa pamoja nao. [14] [f]Wote
tulipokuwa tumeanguka chini, nikasikia
sauti ikisema nami kwa lugha ya Kiebrania,
‘Sauli, Sauli, mbona unanitesa? Ni vigumu
kwako kuupiga teke mchokoo.’

[15] “Nikauliza, ‘Ni nani wewe, Bwana?’

“Naye Bwana akajibu, ‘Ni Mimi Yesu
unayemtesa. [16] [g]Sasa inuka usimame kwa
miguu yako. Nimekutokea ili nikuteue uwe
mtumishi na shahidi wa mambo ambayo
umeyaona, na yale nitakayokuonyesha.
[17] [h]Nitakuokoa kutoka kwa watu wako
na watu wa Mataifa ambao ninakutuma
kwao, [18] [i]uyafumbue macho yao ili wageuke
kutoka gizani waingie nuruni, na kutoka
kwenye nguvu za Shetani wamgeukie
Mungu, ili wapate msamaha wa dhambi na
sehemu miongoni mwa wale waliotakaswa
kwa kuniamini mimi.’

[19] [j]“Hivyo basi, Mfalme Agripa, sikuacha
kuyatii yale maono yaliyotoka mbinguni,
[20] [k]bali niliyatangaza kwanza kwa wale wa
Dameski, kisha Yerusalemu na katika vijiji
vyote vya Uyahudi na pia kwa watu wa
Mataifa, kwamba inawapasa kutubu na
kumgeukia Mungu na kuthibitisha toba
yao kwa matendo yao. [21] [l]Ni kwa sababu
hii Wayahudi walinikamata nilipokuwa
Hekaluni, wakataka kuniua. [22] [m]Hadi leo
nimepata msaada kutoka kwa Mungu, na
hivyo nasimama hapa nikishuhudia kwa
wakubwa na wadogo. Sisemi chochote zaidi
ya yale ambayo manabii na Mose walisema
yatatukia: [23] [n]kwamba Kristo[o] atateswa, na
kwamba yeye atakuwa wa kwanza kufufuka
kutoka kwa wafu, na atatangaza nuru kwa
watu wake na kwa watu wa Mataifa.”

### *Paulo Aeleza Juu Ya Kuhubiri Kwake*

[24] [p]Paulo alipokuwa akifanya utetezi huu,
Festo akasema kwa sauti kubwa, “Paulo,
wewe umerukwa na akili! Kusoma kwingi
kunakufanya uwe kichaa!”

[25] [q]Lakini Paulo akajibu, “Mimi sijarukwa
na akili, mtukufu sana Festo, bali nanena
kweli nikiwa na akili zangu timamu.
[26] [r]Naam, Mfalme anajua kuhusu mambo
haya yote, nami nasema naye kwa uhuru.

[a]**26:7** Yn 1:1; 1The 3:10; 1Tim 5:5
[b]**26:8** Mdo 23:6
[c]**26:9** 1Tim 1:13; Yn 16:2; 15:21
[d]**26:10** Mdo 9:13; 8:3; 9:2, 14, 21; 22:20
[e]**26:11** Mt 10:17
[f]**26:14** Mdo 9:7
[g]**26:16** Eze 2:1; Dan 10:11; Mdo 22:14, 15
[h]**26:17** Yer 1:8, 19; Mdo 9:15
[i]**26:18** Isa 35:5; Za 18:29; Kol 1:13; Lk 24:27; Mdo 2:38; 20:21-32
[j]**26:19** Isa 50:5
[k]**26:20** Mdo 9:19-25; 9:26-29; 22:18-20; 9:15; 13:46; 3:19; Yer 18:11; Mt 3:8
[l]**26:21** Mdo 21:27, 30; 21:31
[m]**26:22** Lk 24:27, 44; Mdo 10:43
[n]**26:23** Kol 1:18; Ufu 1:5; Lk 2:32
[o]23 *Kristo* maana yake ni *Masiya*, yaani *Aliyetiwa mafuta.*
[p]**26:24** Yn 10:20
[q]**26:25** Mdo 23:26
[r]**26:26** Mdo 26:3

Kwa sababu nina hakika kwamba hakuna hata mojawapo ya mambo haya asilolijua, kwa kuwa hayakufanyika mafichoni. 27 Mfalme Agripa, je, unaamini manabii? Najua kuwa unaamini."

28 [a]Agripa akamwambia Paulo, "Je, unanishawishi kwa haraka namna hii niwe Mkristo?"

29 [b]Paulo akasema, "Ikiwa ni kwa haraka au la, namwomba Mungu, si wewe peke yako bali pia wale wote wanaonisikiliza leo, wawe kama mimi nilivyo, kasoro minyororo hii."

30 [c]Baada ya kusema hayo, mfalme akainuka pamoja na mtawala na Bernike na wale waliokuwa wameketi pamoja nao. 31 [d]Walipokuwa wakiondoka, wakaambiana, "Mtu huyu hafanyi jambo lolote linalostahili kufa au kufungwa."

32 [e]Agripa akamwambia Festo, "Mtu huyu angeachwa huru kama hangekuwa amekata rufaa kwa Kaisari."

*Paulo Asafiri Kwenda Rumi*

27 [f]Ilipoamuliwa kwamba tungesafiri kwa njia ya bahari kwenda Italia, Paulo na wafungwa wengine wakakabidhiwa kwa kiongozi mmoja wa askari aliyeitwa Juliasi, aliyekuwa wa Kikosi cha Walinzi wa Kaisari. 2 [g]Tulipanda meli iliyotoka Adramitio, iliyokuwa inakaribia kusafiri kwenda kwenye bandari zilizopo pwani ya Asia, tukaanza safari yetu tukiwa pamoja na Aristarko, Mmakedonia kutoka Thesalonike.

3 [h]Kesho yake tukatia nanga Sidoni, naye Juliasi akamfanyia wema Paulo, akamruhusu aende kwa rafiki zake ili wamtimizie mahitaji yake. 4 [i]Kutoka huko tukaingia baharini tena na tukapita upande wa chini wa kisiwa cha Kipro kwa sababu upepo ulikuwa wa mbisho. 5 [j]Baada ya sisi kuvuka bahari iliyoko upande wa Kilikia na Pamfilia, tukafika Mira huko Likia. 6 [k]Huko yule kiongozi wa askari akapata meli ya Iskanderia ikielekea Italia, akatupandisha humo. 7 [l]Tukasafiri polepole kwa siku nyingi na kwa shida, hatimaye tukafika karibu na Nido. Kwa kuwa upepo wa mbisho ulituzuia tusiweze kushika mwelekeo tuliokusudia, tukapita chini ya Krete mkabala na Salmone. 8 Tukaambaa na pwani kwa shida, tukafika sehemu iitwayo Bandari Nzuri, karibu na mji wa Lasea.

9 [m]Muda mwingi ulikuwa umepotea na kusafiri baharini kulikuwa hatari kwa sababu wakati huu ulikuwa baada ya siku za kufunga. Hivyo Paulo akawaonya akasema, 10 [n]"Mabwana, naona kuwa hii safari ni yenye maafa na ya kuleta hasara kubwa kwa meli na shehena, pia kwa maisha yetu." 11 Lakini badala ya yule kiongozi wa askari kusikiliza yale Paulo aliyosema, akafuata zaidi ushauri wa nahodha na mwenye meli. 12 [o]Kwa kuwa ile bandari ilikuwa haifai kukaa wakati wa majira ya baridi, wengi wakashauri kwamba tuendelee na safari wakitarajia kufika Foinike na kukaa huko kwa majira ya baridi. Hii ilikuwa bandari iliyoko katika kisiwa cha Krete ikikabili upande wa kusini-magharibi na kaskazini-magharibi.

*Dhoruba Baharini*

13 Upepo mtulivu ulipoanza kuvuma toka kusini, wakadhani kuwa wangeweza kufikia lengo lao, hivyo wakang'oa nanga na kusafiri wakipita kandokando ya pwani ya kisiwa cha Krete. 14 [p]Lakini baada ya muda mfupi ikavuma tufani kubwa iitwayo "Eurakilo" toka kisiwa cha Krete. 15 Meli ikapigwa na dhoruba na haikuweza kushindana na ule upepo, tukarudishwa baharini upepo ulikokuwa

[a]**26:28** Mdo 11:26
[b]**26:29** Mdo 21:33
[c]**26:30** Mdo 25:23
[d]**26:31** Mdo 23:9
[e]**26:32** Mdo 28:18; 25:11
[f]**27:1** Mdo 25:12, 25
[g]**27:2** Mdo 19:29
[h]**27:3** Mdo 24:23; 28:16
[i]**27:4** Mdo 27:7
[j]**27:5** Mdo 6:9; 2:10
[k]**27:6** Mdo 28:11; 18:2; 25:12, 25
[l]**27:7** Tit 1:5
[m]**27:9** Law 16:29-31; 23:27-29; Hes 29:7
[n]**27:10** Mdo 27:21
[o]**27:12** Mdo 27:7
[p]**27:14** Mk 4:37

unaelekea. 16 [a]Hatimaye tukisafiri kupita
chini ya kisiwa kidogo kiitwacho Kauda,
ambapo kwa kuwa tulikuwa tumekingiwa
upepo na hicho kisiwa, tuliweza kwa
shida kuifunga mashua ya kuokolea watu.
17 [b]Watu walipokwisha kuivuta mashua
hiyo na kuiingiza katika meli, waliifunga
kwa kamba chini ya meli yenyewe ili
kuzishikanisha pamoja. Wakiogopa
kupelekwa kwenye mchanga karibu na
pwani ya Sirti, wakashusha matanga
wakaiacha meli isukumwe na huo upepo.
18 [c]Tulikuwa tunapigwa na dhoruba kwa
nguvu, kiasi kwamba kesho yake walianza
kutupa shehena toka melini. 19 [d]Siku ya
tatu, wakatupa vyombo vya meli baharini
kwa mikono yao wenyewe. 20 Kulipokuwa
hakuna kuonekana kwa jua wala nyota kwa
siku nyingi, nayo dhoruba ikiwa inaendelea
kuwa kali, hatimaye tulikata kabisa tamaa
ya kuokoka.
21 [e]Baada ya watu kukaa siku nyingi bila
kula chakula, Paulo akasimama katikati
yao akasema, “Enyi watu, iliwapasa
kunisikiliza na kuacha kusafiri baharini
kutoka Krete, ndipo ninyi mngekuwa
mmejinusuru na uharibifu huu na hasara
hii. 22 [f]Sasa ninawasihi sana, jipeni moyo
mkuu kwa kuwa hakuna hata mmoja
wenu atakayepoteza maisha yake, ila
meli itaangamia. 23 [g]Jana usiku, malaika
wa Mungu yule ambaye mimi ni wake na
ambaye ninamwabudu alisimama karibu
nami, 24 [h]naye akasema, ‘Paulo usiogope,
kwa kuwa ni lazima usimame mbele ya
Kaisari, naye Mungu amekupa kwa neema
uhai wa wote wanaosafiri pamoja nawe.
25 [i]Hivyo jipeni moyo, enyi watu, kwa kuwa
ninamwamini Mungu kwamba yatakuwa
kama vile alivyoniambia.’ 26 [j]Lakini hata
hivyo meli yetu itakwama kwenye kisiwa
fulani.”

*Maangamizi Ya Meli*

27 Usiku wa kumi na nne ulipofika,
tulikuwa bado tunasukumwa na upepo
katika Bahari ya Adria. Ilipokuwa yapata
usiku wa manane, mabaharia wakahisi
kwamba walikuwa wanakaribia nchi kavu.
28 Kwa hiyo wakapima kina cha maji na
kukuta kilikuwa pima ishirini,[k] baada
ya kuendelea mbele kidogo wakapima
tena wakapata kina cha pima kumi na
tano.[l] 29 Wakiogopa kwamba meli yetu
ingegonga kwenye miamba, wakashusha
nanga nne za nyuma ya meli, wakawa
wanaomba kupambazuke. 30 [m]Katika jaribio
la kutoroka kutoka kwenye meli, mabaharia
wakashusha mashua ya kuokolea watu
baharini, wakijifanya kwamba wanakwenda
kushusha nanga za omo.[n] 31 [o]Ndipo Paulo
akamwambia yule jemadari na askari,
“Hawa watu wasipobaki katika meli,
hamtaweza kuokoka.” 32 Hivyo basi wale
askari wakakata kamba zilizoshikilia ile
mashua ya kuokolea watu kwenye meli,
wakaiacha ianguke humo baharini.
33 [p]Kabla ya mapambazuko, Paulo
akawasihi watu wote wale chakula akisema,
“Leo ni siku ya kumi na nne mmekuwa
katika wasiwasi mkiwa mmefunga na bila
kula chochote. 34 [q]Kwa hiyo nawasihi mle
chakula, kwa maana itawasaidia ili mweze
kuishi. Kwa kuwa hakuna hata mmoja wenu
atakayepoteza unywele hata mmoja kutoka
kichwani mwake.” 35 [r]Baada ya kusema
maneno haya, Paulo akachukua mkate,
akamshukuru Mungu mbele yao wote,
akaumega akaanza kula. 36 [s]Ndipo wote
wakatiwa moyo, wakaanza kula chakula.

---

[a]**27:16** Mdo 27:30
[b]**27:17** Mdo 27:26, 39
[c]**27:18** Yn 1:5; Mdo 27:19, 38; Yn 1:5
[d]**27:19** Yon 1:5
[e]**27:21** Mdo 27:10; 27:7
[f]**27:22** Mdo 7:25, 36
[g]**27:23** Mdo 5:19; Rum 1:9; 2Tim 4:19
[h]**27:24** Mdo 23:11
[i]**27:25** Rum 4:20, 21
[j]**27:26** Mdo 28:1
[k]28 Pima 20 ni kama mita 40.
[l]28 Pima 15 ni kama mita 30.
[m]**27:30** Mdo 27:16
[n]30 Omo hapa maana yake ni sehemu ya mbele ya meli, yaani gubeti.
[o]**27:31** Mdo 27:24
[p]**27:33** Mdo 27:27
[q]**27:34** Mt 10:30
[r]**27:35** Mt 14:19
[s]**27:36** Mdo 27:22, 25

37 [a]Ndani ya meli tulikuwa jumla ya watu
276. 38 [b]Baada ya watu wote kula chakula
cha kutosha, wakapunguza uzito wa meli
kwa kutupa ngano baharini.
39 [c]Kulipopambazuka, mabaharia
hawakuitambua ile nchi, lakini waliona
ghuba yenye ufuko wa mchanga,
ambako waliamua kuipweleza meli kama
ingewezekana. 40 Kwa hiyo wakatupa nanga
zote na kuziacha baharini, na wakati huo huo
wakalegeza kamba zilizokuwa zikishikilia
usukani wa meli. Kisha wakatweka tanga
la mbele lishike upepo na kuisukuma
meli kuelekea pwani. 41 [d]Lakini wakafika
mahali ambapo bahari mbili zinakutana,
wakaipweleza meli ufuoni, omo ikakwama
sana, ikawa haiwezi kuondolewa, lakini
sehemu ya shetri[e] ikavunjika vipande
vipande kwa kule kupiga kwa mawimbi
yenye nguvu.
42 Wale askari wakapanga kuwaua
wale wafungwa ili kuzuia hata mmoja
wao asiogelee na kutoroka. 43 Lakini yule
jemadari alitaka kuokoa maisha ya Paulo,
basi akawazuia askari wasitekeleze mpango
wao. Akaamuru wale wanaoweza kuogelea
wajitupe baharini kwanza, waogelee mpaka
nchi kavu. 44 Waliosalia wangefika nchi
kavu kwa kutumia mbao au vipande vya
meli iliyovunjika, hivyo ikatimia kwamba
wote wakaokoka na kufika nchi kavu
salama.

*Paulo Kisiwani Malta*

28 [f]Baada ya kufika nchi kavu salama,
ndipo tukafahamu kwamba jina la kile
kisiwa ni Malta. 2 [g]Wenyeji wa kile kisiwa
wakatufanyia ukarimu usio wa kawaida.
Waliwasha moto na kutukaribisha sisi
sote kwa sababu mvua ilikuwa inanyesha
na kulikuwa na baridi. 3 Paulo alikuwa
amekusanya mzigo wa kuni na alipokuwa
anaweka kwenye moto kwa ajili ya joto,
nyoka mwenye sumu akatoka humo na
kujisokotea mkononi mwake. 4 [h]Wale
wenyeji wa kile kisiwa walipomwona yule
nyoka akining'inia mkononi mwa Paulo,
wakaambiana, "Huyu mtu lazima awe ni
muuaji, ingawa ameokoka kutoka baharini,
haki haijamwacha aishi." 5 [i]Lakini Paulo
akamkung'utia yule nyoka ndani ya moto
wala yeye hakupata madhara yoyote.
6 [j]Watu walikuwa wanangoja avimbe au
aanguke ghafula na kufa. Lakini baada ya
kungoja kwa muda mrefu na kuona kwamba
hakuna chochote kisicho cha kawaida
kilichomtokea, wakabadili mawazo yao
na kuanza kusema kwamba yeye ni mungu.
7 Basi karibu na sehemu ile, palikuwa na
shamba kubwa la mtu mmoja kiongozi wa
kile kisiwa, aliyeitwa Publio. Alitupokea
na akatuhudumia kwa ukarimu mkubwa
kwa muda wa siku tatu. 8 [k]Baba yake
Publio alikuwa mgonjwa kitandani, akiwa
anaumwa homa na kuhara damu. Paulo
akaingia ndani ili kumwona na baada ya
maombi, akaweka mikono juu yake na
kumponya. 9 Jambo hili lilipotukia, watu
wote wa kisiwa kile waliokuwa wagonjwa
wakaja, nao wakaponywa. 10 [l]Wakatupa
heshima nyingi, nasi tulipokuwa tayari
kusafiri kwa njia ya bahari, wakapakia
melini vitu vyote tulivyokuwa tunavihitaji.

*Paulo Awasili Rumi*

11 [m]Miezi mitatu baadaye tukaanza
safari kwa meli iliyokuwa imetia nanga
kwenye kisiwa hicho kwa ajili ya majira
ya baridi. Hii ilikuwa meli ya Iskanderia
yenye alama ya miungu pacha waitwao
Kasta na Poluksi. 12 Kituo chetu cha kwanza
kilikuwa Sirakusa na tukakaa huko siku
tatu. 13 Kisha tukang'oa nanga, tukafika
Regio. Siku iliyofuata, upepo mkali wa
kusi ukavuma, na siku ya pili yake tukafika

[a]**27:37** Mdo 2:41; 7:14; Rum 13:1; 1Pet 3:20
[b]**27:38** Yn 1:5
[c]**27:39** Mdo 28:1
[d]**27:41** 2Kor 11:25
[e]41 Shetri ni sehemu ya nyuma ya meli ambayo pia huitwa tezi.
[f]**28:1** Mdo 16:10; 27:26, 39
[g]**28:2** Mdo 27:3; 2Kor 11:27
[h]**28:4** Mk 16:18; Lk 13:2, 4
[i]**28:5** Lk 10:19
[j]**28:6** Mdo 14:11
[k]**28:8** Yak 5:14, 15; Mdo 9:40
[l]**28:10** Mt 15:6; 1Tim 5:17; Za 15:4
[m]**28:11** Mdo 27:6

Puteoli. [14] [a]Huko tukawakuta ndugu, nasi
tukakaribishwa tukae nao kwa siku saba.
Hivyo tukaendelea na safari mpaka Rumi.
[15] [b]Ndugu wa huko Rumi waliposikia
habari zetu, walikuja mpaka Soko la Apio
na mahali paitwapo Mikahawa Mitatu
kutulaki. Paulo alipowaona, alimshukuru
Mungu akatiwa moyo. [16] [c]Tulipofika Rumi,
Paulo aliruhusiwa kuishi peke yake akiwa
na askari wa kumlinda.

*Paulo Ahubiri Rumi Chini Ya Ulinzi*

[17] [d]Siku tatu baadaye Paulo akawaita
pamoja viongozi wa Kiyahudi.
Walipokwisha kukusanyika akawaambia,
"Ndugu zangu, ingawa sikufanya jambo
lolote dhidi ya watu wetu au dhidi ya desturi
za baba zetu, lakini nilikamatwa huko
Yerusalemu nikakabidhiwa kwa Warumi.
[18] [e]Wao walipokwisha kunihoji, wakataka
kuniachia huru kwa sababu hawakuona
kosa lolote nililolifanya linalostahili adhabu
ya kifo. [19] [f]Lakini Wayahudi walipopinga
uamuzi huo, nililazimika kukata rufaa
kwa Kaisari, ingawa sikuwa na lalamiko
lolote juu ya taifa langu. [20] [g]Basi hii ndiyo
sababu nimewatumania, ili niseme nanyi.
Kwa kuwa ni kwa ajili ya tumaini la Israeli
nimefungwa kwa minyororo."

[21] [h]Wakamjibu, "Hatujapokea barua
zozote kutoka Uyahudi zinazokuhusu,
wala hapana ndugu yeyote aliyekuja hapa
ambaye ametoa taarifa au kuzungumza
jambo lolote baya juu yako. [22] [i]Lakini
tungependa kusikia kutoka kwako
unalofikiri kwa sababu tunajua kwamba
kila mahali watu wanazungumza mabaya
kuhusu jamii hii."

[23] [j]Baada ya kupanga siku ya kuonana
naye, watu wengi wakaja kuanzia asubuhi
hadi jioni akawaeleza na kutangaza kuhusu
Ufalme wa Mungu akijaribu kuwahadithia
juu ya Yesu kutoka Sheria ya Mose na
kutoka Manabii. [24] [k]Baadhi wakasadiki yale
aliyosema, lakini wengine hawakuamini.
[25] Hivyo hawakukubaliana, nao walipokuwa
wanaondoka, Paulo akatoa kauli moja zaidi:
"Roho Mtakatifu alinena kweli na baba
zenu aliposema mambo yale yaliyomhusu
Bwana Yesu kwa kinywa cha nabii Isaya
kwamba:

[26] [l]" 'Nenda kwa watu hawa na useme,
"Hakika mtasikiliza lakini
hamtaelewa;
na pia mtatazama, lakini
hamtaona."
[27] [m]Kwa kuwa mioyo ya watu hawa
imekuwa migumu;
hawasikii kwa masikio yao,
na wamefumba macho yao.
Wasije wakaona kwa macho yao,
na wakasikiliza kwa masikio yao,
wakaelewa kwa mioyo yao,
na kugeuka nami nikawaponya.'

[28] [n]"Basi na ijulikane kwenu kwamba,
huu wokovu wa Mungu umepelekwa
kwa watu wa Mataifa, nao watasikiliza."
[ [29] Naye akiisha kusema maneno haya,
Wayahudi wakaondoka wakiwa na hoja
nyingi miongoni mwao.]

[30] Kwa miaka miwili mizima Paulo alikaa
huko kwa nyumba aliyokuwa amepanga.
Akawakaribisha wote waliokwenda
kumwona. [31] [o]Akahubiri Ufalme wa Mungu
na kufundisha mambo yale yaliyomhusu
Bwana Yesu Kristo, kwa ujasiri wote na
bila kizuizi chochote.

---

[a]**28:14** Mdo 1:16
[b]**28:15** Mdo 1:16
[c]**28:16** Mdo 24:23; 27:3
[d]**28:17** Mdo 25:2; 22:5; 25:8; 6:14
[e]**28:18** Mdo 22:24; 26:31, 32; 23:9
[f]**28:19** Mdo 25:11; 26:32
[g]**28:20** Mdo 26:6, 7; 21:33
[h]**28:21** Mdo 22:5
[i]**28:22** Mdo 24:5, 14
[j]**28:23** Mt 3:2; Mdo 19:8; 17:3; 8:35
[k]**28:24** Mdo 14:4
[l]**28:26** Isa 6:9; Yer 5:21; Eze 12:2; Mt 13:14, 15; Mk 4:12; Lk 8:10; Yn 12:40; Rum 11:8
[m]**28:27** Za 119:70; Isa 6:9, 10
[n]**28:28** Lk 2:30; Mdo 13:46
[o]**28:31** Mdo 4:29; Mt 4:23; Mdo 4:29; 28:23; Mt 4:23; Mdo 4:23; 4:23; 4:31; Efe 6:19

# WARUMI

1 [a]Paulo, mtumishi wa Kristo Yesu,
aliyeitwa kuwa mtume na kutengwa
kwa ajili ya Injili ya Mungu, [2] [b]Injili ambayo
Mungu alitangulia kuiahidi kwa vinywa vya
manabii wake katika Maandiko Matakatifu,
[3] [c]yaani, Injili inayomhusu Mwanawe, yeye
ambaye kwa uzao wa mwili alikuwa mzao
wa Daudi, [4] [d]na ambaye kwa uwezo wa
Roho wa utakatifu alidhihirishwa kuwa
Mwana wa Mungu kwa ufufuo wake kutoka
kwa wafu, yaani, Yesu Kristo, Bwana
wetu. [5] [e]Kwa kupitia kwake na kwa ajili
ya Jina lake, tumepokea neema na utume
ili kuwaita watu miongoni mwa watu wa
mataifa yote, waje kwenye utii utokanao
na imani. [6] [f]Ninyi nyote pia mko miongoni
mwa watu walioitwa ili mpate kuwa mali
ya Yesu Kristo.

[7] [g]Kwa wote walioko Rumi wapendwao
na Mungu na kuitwa kuwa watakatifu:

Neema na amani itokayo kwa Mungu
Baba yetu na kwa Bwana wetu Yesu Kristo
iwe nanyi.

*Maombi Na Shukrani*

[8] [h]Kwanza kabisa, namshukuru Mungu
wangu kwa njia ya Yesu Kristo kwa ajili
yenu nyote, kwa sababu imani yenu
inatangazwa duniani kote. [9] [i]Kwa maana
Mungu ninayemtumikia kwa moyo wangu
wote katika kuhubiri Injili ya Mwanawe,
ni shahidi wangu jinsi ninavyowakumbuka
[10] [j]katika maombi yangu siku zote, nami
ninaomba kwamba hatimaye sasa kwa
mapenzi ya Mungu, njia ipate kufunguliwa
kwa ajili yangu ili nije kwenu.

[11] [k]Ninatamani sana kuwaona ili nipate
kuweka juu yenu karama za rohoni ili
mwe imara, [12] [l]au zaidi, ninyi pamoja nami
tuweze kutiana moyo katika imani sisi kwa
sisi. [13] [m]Ndugu zangu, napenda mfahamu
kwamba mara nyingi nimekusudia kuja
kwenu (ingawa mpaka sasa nimezuiliwa),
ili nipate kuvuna mavuno miongoni mwenu
kama nilivyovuna miongoni mwa wengine
ambao ni watu wa Mataifa wasiomjua
Mungu.

[14] [n]Mimi ni mdeni kwa Wayunani na kwa
wasio Wayunani, kwa wenye hekima na
kwa wasio na hekima. [15] [o]Ndiyo sababu
ninatamani sana kuihubiri Injili kwenu pia
ninyi mlioko Rumi.

[16] [p]Mimi siionei haya Injili ya Kristo
kwa maana ni uweza wa Mungu uletao
wokovu kwa kila aaminiye, kwanza kwa
Myahudi na kwa Myunani pia. [17] [q]Kwa
maana katika Injili haki itokayo kwa Mungu
imedhihirishwa, haki ile iliyo kwa njia ya
imani hadi imani. Kama ilivyoandikwa:
“Mwenye haki ataishi kwa imani.”

*Ghadhabu Ya Mungu Kwa Wanadamu*

[18] Ghadhabu ya Mungu imedhihirishwa
kutoka mbinguni dhidi ya uasi wote na
uovu wa wanadamu ambao huipinga
kweli kwa uovu wao, [19] [r]kwa maana yote
yanayoweza kujulikana kumhusu Mungu
ni dhahiri kwao, kwa sababu Mungu
mwenyewe ameyadhihirisha kwao. [20] [s]Kwa
maana tangu kuumbwa kwa ulimwengu,

---

[a]**1:1** 1Kor 1:1; Mdo 9:15; 1The 2:8, 9; 1Pet 4:17
[b]**1:2** Gal 3:8; Tit 1:2; Rum 16:25, 26; Mdo 26:6; 3:21; Mt 4:3
[c]**1:3** Yn 1:14; Rum 9:5
[d]**1:4** Mt 4:3; Mdo 2:24; 1Kor 1:2; Mdo 13:33
[e]**1:5** Mdo 9:15; 6:7; Rum 16:27
[f]**1:6** Yud 1; Ufu 17:14
[g]**1:7** Rum 8:39; 1The 1:4; Efe 1:2; Tit 1:4
[h]**1:8** Efe 1:16; 1The 2:13; Rum 10:18; 16:19
[i]**1:9** 2Tim 1:1; Yer 42:5; Gal 1:20
[j]**1:10** Rum 15:32; Mdo 19:21; Rum 15:23, 32; 1Sam 12:23; Lk 18:1; Efe 1:16; Flp 1:4; Kol 1:9; 2The 1:11; 2Tim 1:3; Mdo 18:21; Rum 15:32
[k]**1:11** Rum 15:23; 1:7; Mdo 28:31
[l]**1:12** 2Pet 1:1; Tit 1:4
[m]**1:13** Rum 15:22, 23; Yn 15:16; 1The 2:18; Flp 4:17; Mdo 13:23; 16:7
[n]**1:14** 1Kor 9:16
[o]**1:15** Rum 15:20
[p]**1:16** 2Tim 1:8; 1Kor 1:18; Mdo 3:26; 13:26; Rum 2:9, 10
[q]**1:17** Rum 3:21; Flp 3:9; Hab 2:4
[r]**1:19** Mdo 14:17; 17:24-28; Yn 1:9
[s]**1:20** Za 19:1-6; Ebr 11:3; Ay 12:7-9; Rum 2:1

asili ya Mungu asiyeonekana kwa macho,
yaani, uweza wake wa milele na asili
yake ya Uungu, imeonekana waziwazi,
ikitambuliwa kutokana na yale aliyoyafanya
ili wanadamu wasiwe na udhuru.
[21] [a]Kwa maana ingawa walimjua Mungu,
hawakumtukuza yeye kama ndiye Mungu
wala hawakumshukuru, bali fikira zao
zimekuwa batili na mioyo yao ya ujinga
ikatiwa giza. [22] [b]Ingawa walijidai kuwa
wenye hekima, wakawa wajinga [23] [c]na
kubadili utukufu wa Mungu aishiye milele
kwa sanamu zilizofanywa zifanane na
mwanadamu ambaye hufa, na mfano wa
ndege, wanyama na viumbe vitambaavyo.
[24] [d]Kwa hiyo, Mungu akawaacha wazifuate
tamaa mbaya za mioyo yao katika uasherati,
hata wakavunjiana heshima miili yao wao
kwa wao. [25] [e]Kwa sababu waliibadili kweli
ya Mungu kuwa uongo, wakaabudu na
kutumikia kiumbe badala ya Muumba,
ahimidiwaye milele! Amen.
[26] [f]Kwa sababu hii, Mungu aliwaacha
wavunjiane heshima kwa kufuata
tamaa zao za aibu. Hata wanawake wao
wakabadili matumizi ya asili ya miili yao
wakaitumia isivyokusudiwa. [27] [g]Vivyo hivyo
wanaume pia wakiacha matumizi ya asili ya
wanawake wakawakiana tamaa wao kwa
wao. Wanaume wakafanyiana matendo ya
aibu na wanaume wengine nao wakapata
katika maisha yao adhabu iliyowastahili
kwa ajili ya upotovu wao.
[28] [h]Nao kwa kuwa hawakuona umuhimu
wa kudumisha ufahamu wa Mungu, yeye
akawaachilia wafuate akili za upotovu,
watende mambo yale yasiyostahili
kutendwa. [29] [i]Wakiwa wamejawa na
udhalimu wa kila namna, uasherati, uovu,
tamaa mbaya na hila. Wamejawa na
husuda, uuaji, ugomvi, udanganyifu, hadaa
na nia mbaya. Wao pia ni wasengenyaji,
[30] [j]wasingiziaji, wanaomchukia Mungu,
wajeuri, wenye kiburi na majivuno, wenye
hila, wasiotii wazazi wao, [31] [k]wajinga,
wasioamini, wasio na huruma na wakatili.
[32] [l]Ingawa wanafahamu sheria ya haki ya
Mungu kwamba watu wanaofanya mambo
kama hayo wanastahili mauti, si kwamba
wanaendelea kutenda hayo tu, bali pia
wanakubaliana na wale wanaoyatenda.

*Hukumu Ya Mungu*

2 [m]Kwa hiyo huna udhuru wowote, wewe
utoaye hukumu kwa mwingine, kwa
maana katika jambo lolote unalowahukumu
wengine, unajihukumu wewe mwenyewe
kwa sababu wewe unayehukumu unafanya
mambo hayo hayo. [2] [n]Basi tunajua kwamba
hukumu ya Mungu dhidi ya wale wafanyao
mambo kama hayo ni ya kweli. [3] Hivyo
wewe mwanadamu, utoapo hukumu juu
yao na bado unafanya mambo yale yale,
unadhani utaepuka hukumu ya Mungu?
[4] [o]Au waudharau wingi wa wema, ustahimili
na uvumilivu wake, bila kujua kuwa wema
wa Mungu wakuelekeza kwenye toba?
[5] [p]Lakini kwa sababu ya ukaidi wenu na
mioyo yenu isiyotaka kutubu, mnajiwekea
akiba ya ghadhabu dhidi yenu wenyewe
kwa siku ile ya ghadhabu ya Mungu, wakati
hukumu yake ya haki itakapodhihirishwa.
[6] [q]Kwa maana Mungu atamlipa kila mtu
sawasawa na matendo yake. [7] [r]Wale ambao
kwa kuvumilia katika kutenda mema
hutafuta utukufu, heshima na maisha
yasiyoharibika, Mungu atawapa uzima
wa milele. [8] [s]Lakini kwa wale watafutao
mambo yao wenyewe na wale wanaokataa

[a]**1:21** Mwa 8:21; Efe 4:18; Ufu 14:7
[b]**1:22** Kol 1:20, 27; 3:18, 19
[c]**1:23** Yer 2:11; Mdo 17:29
[d]**1:24** Za 81:12; Efe 4:19; 1Pet 4:3
[e]**1:25** Isa 44:20; Yer 13:25; 16:19, 20; Rum 9:5; 2Kor 11:31
[f]**1:26** Efe 4:19; 1The 4:5; Law 18:22, 23
[g]**1:27** Law 20:13; 1Kor 6:18
[h]**1:28** Rum 1:24-26; Efe 5:4
[i]**1:29** 3Yn 10
[j]**1:30** 2Tim 3:2
[k]**1:31** 2Tim 3:3
[l]**1:32** Rum 6:23; Za 50:18; Lk 11:48
[m]**2:1** Rum 1:20; 2Sam 12:5-7; Mt 7:12
[n]**2:2** 2Sam 12:5-7; Mt 7:12
[o]**2:4** Efe 3:8, 16; Kol 2:2; Rum 11:22; 3:25; Kut 34:6
[p]**2:5** 1Pet 3:20; 2Pet 3:9
[q]**2:6** Za 62:12; Mt 16:27
[r]**2:7** 1Kor 15:53, 54; 2Tim 1:10
[s]**2:8** 2The 2:12

kweli na kuzifuata njia mbaya, kutakuwa na ghadhabu na hasira ya Mungu. 9 [a]Kutakuwa na taabu na dhiki kwa kila mmoja atendaye maovu, Myahudi kwanza na mtu wa Mataifa pia, 10 [b]bali utukufu, heshima na amani kwa ajili ya kila mmoja atendaye mema, kwa Myahudi kwanza, kisha kwa mtu wa Mataifa. 11 [c]Kwa maana Mungu hana upendeleo.

12 [d]Watu wote waliotenda dhambi pasipo sheria wataangamia pasipo sheria, nao wote wale waliotenda dhambi chini ya sheria watahukumiwa kwa sheria. 13 [e]Kwa maana si wale wanaoisikia sheria ambao ni wenye haki mbele za Mungu, bali ni wale wanaoitii sheria ndio watakaohesabiwa haki. 14 [f](Naam, wakati wa watu wa Mataifa, ambao hawana sheria, wanapofanya kwa asili mambo yatakiwayo na sheria, wao ni sheria kwa nafsi zao wenyewe, hata ingawa hawana sheria. 15 [g]Wao wanaonyesha kwamba lile linalotakiwa na sheria limeandikwa kwenye mioyo yao, ambayo pia dhamiri zao zikiwashuhudia, nayo mawazo yao yenye kupingana yatawashtaki au kuwatetea.) 16 [h]Hili litatukia siku hiyo Mungu atakapozihukumu siri za wanadamu kwa njia ya Yesu Kristo, kama isemavyo Injili yangu.

### *Wayahudi Na Sheria*

17 [i]Tazama, wewe ukiwa unaitwa Myahudi na kuitegemea sheria na kujisifia uhusiano wako na Mungu, 18 [j]kama unajua mapenzi ya Mungu na kukubali lililo bora kwa sababu umefundishwa na hiyo sheria, 19 [k]kama unatambua kuwa wewe ni kiongozi wa vipofu, na mwanga kwa wale walio gizani, 20 [l]mkufunzi wa wajinga na mwalimu wa watoto wachanga, kwa kuwa una maarifa ya kweli katika hiyo sheria, 21 [m]basi wewe, uwafundishaye wengine, mbona hujifunzi mwenyewe? Wewe uhubiriye kwamba mtu asiibe, wewe mwenyewe waiba? 22 [n]Wewe usemaye mtu asizini, wewe mwenyewe wazini? Wewe uchukiaye miungu ya sanamu, wafanya jambo la kumchukiza katika mahekalu? 23 Wewe ujivuniaye sheria, wamwaibisha Mungu kwa kuvunja sheria? 24 [o]Kama ilivyoandikwa, "Kwa ajili yenu ninyi, Jina la Mungu linatukanwa miongoni mwa watu wa Mataifa."

25 [p]Kutahiriwa kuna thamani ikiwa unatii sheria, lakini kama unavunja sheria, kutahiriwa kwako kumekuwa kutokutahiriwa. 26 [q]Hivyo, ikiwa wale wasiotahiriwa wanatimiza mambo ambayo sheria inataka, je, kutokutahiriwa kwao hakutahesabiwa kuwa sawa na kutahiriwa? 27 [r]Ndipo wale ambao hawakutahiriwa kimwili lakini wanaitii sheria watawahukumu ninyi, ambao ingawa mmetahiriwa na kuijua sana sheria ya Mungu iliyoandikwa, lakini mwaivunja.

28 [s]Kwa maana mtu si Myahudi kwa vile alivyo kwa nje, wala tohara ya kweli si kitu cha nje au cha kimwili. 29 [t]Lakini mtu ni Myahudi alivyo ndani, nayo tohara ya kweli ni jambo la moyoni, ni la Roho, wala si la sheria iliyoandikwa. Mtu wa namna hiyo hapokei sifa kutoka kwa wanadamu bali kwa Mungu.

### *Uaminifu Wa Mungu*

3 Basi kuna faida gani kuwa Myahudi? Au kuna thamani gani katika tohara?

[a]**2:9** 1Pet 4:17; Rum 1:16; 3:9; Za 32:10
[b]**2:10** Rum 1:16; 2:9
[c]**2:11** Mdo 10:34; 1Pet 1:17
[d]**2:12** 1Kor 9:20, 21; Gal 4:21
[e]**2:13** Yak 1:22, 23, 25
[f]**2:14** Mdo 10:34
[g]**2:15** Mhu 12:14; 1Kor 4:5; Mdo 10:42; Rum 16:25; 2Tim 2:8
[h]**2:16** Mhu 12:14; 1Kor 4:5; Mdo 10:42; Rum 16:25; 2Tim 2:8
[i]**2:17** Yer 8:8; Yn 5:45
[j]**2:18** Flp 1:10; Kum 4:8; Za 147:19, 20; Flp 1:10
[k]**2:19** Mt 15:14; Lk 18:9
[l]**2:20** 2Tim 1:13; 3:5
[m]**2:21** Mt 23:3, 4; Za 50:16
[n]**2:22** Mdo 19:32; Mal 3:8
[o]**2:24** Isa 52:5; 2Pet 2:2
[p]**2:25** Gal 5:3; Yer 4:4; 9:25, 26
[q]**2:26** Rum 8:4; 1Kor 7:19
[r]**2:27** Mt 12:41, 42
[s]**2:28** Mt 3:9; Yn 8:39
[t]**2:29** Flp 3:3; Kol 2:11; Rum 7:6; 2Kor 3:6; Yn 12:43; Gal 1:10

2 [a]Kuna faida kubwa kwa kila namna!
Kwanza kabisa, Wayahudi wamekabidhiwa
lile Neno halisi la Mungu. 3 [b]Ingekuwaje
kama wengine hawakuwa na imani? Je,
kutokuamini kwao kungebatilisha uaminifu
wa Mungu? 4 [c]La hasha! Mungu na aonekane
mwenye haki, na kila mwanadamu kuwa
mwongo, kama ilivyoandikwa:

"Ili uthibitike kuwa wa kweli
unaponena,
na ukashinde utoapo hukumu."

5 [d]Ikiwa uovu wetu unathibitisha haki
ya Mungu waziwazi, tuseme nini basi?
Je, Mungu kuileta ghadhabu yake juu
yetu ni kwamba yeye si mwenye haki?
(Nanena kibinadamu.) 6 [e]La hasha! Kama
hivyo ndivyo ilivyo, Mungu angehukumuje
ulimwengu? 7 [f]Mtu aweza kuuliza, "Kama
uongo wangu unasaidia kuonyesha kweli
ya Mungu na kuzidisha utukufu wake, kwa
nini basi mimi nahukumiwa kuwa mwenye
dhambi?" 8 [g]Nasi kwa nini tusiseme,
kama wengine wanavyotusingizia kuwa
tunasema, "Tutende maovu ili mema yapate
kuja?" Wao wanastahili hukumu yao.

*Wote Wametenda Dhambi*

9 [h]Tusemeje basi? Je, sisi ni bora kuwaliko
wao? La hasha! Kwa maana tumekwisha
kuhakikisha kwa vyovyote kwamba
Wayahudi na watu wa Mataifa wote
wako chini ya nguvu ya dhambi. 10 [i]Kama
ilivyoandikwa:

"Hakuna mwenye haki, hakuna hata
mmoja.
11 Hakuna hata mmoja mwenye
ufahamu,
hakuna hata mmoja amtafutaye
Mungu.
12 [j]Wote wamepotoka,
wote wameoza pamoja;
hakuna atendaye mema,
naam, hakuna hata mmoja."
13 [k]"Makoo yao ni makaburi wazi;
kwa ndimi zao wao hufanya
udanganyifu."
"Sumu ya nyoka iko midomoni
mwao."
14 [l]"Vinywa vyao vimejaa laana na
uchungu."
15 [m]"Miguu yao ina haraka kumwaga
damu;
16 maangamizi na taabu viko katika
njia zao,
17 [n]wala njia ya amani hawaijui."
18 [o]"Hakuna hofu ya Mungu machoni
pao."

19 [p]Basi tunajua ya kwamba chochote
sheria inachosema, inawaambia wale walio
chini ya sheria ili kila kinywa kinyamazishwe
na ulimwengu wote uwajibike kwa Mungu.
20 [q]Kwa hiyo hakuna binadamu hata mmoja
atakayehesabiwa haki mbele za Mungu
kwa matendo ya sheria, kwa maana sheria
hutufanya tuitambue dhambi.

*Haki Kwa Njia Ya Imani*

21 [r]Lakini sasa, haki itokayo kwa Mungu
imedhihirishwa pasipo sheria, ambayo
Sheria na Manabii wanaishuhudia. 22 [s]Haki
hii itokayo kwa Mungu hupatikana kwa
Yesu Kristo kwa wote wamwaminio. Kwa
maana hapo hakuna tofauti, 23 [t]kwa kuwa
wote wametenda dhambi na kupungukiwa
na utukufu wa Mungu, 24 [u]wanahesabiwa
haki bure kwa neema yake kwa njia ya

[a]**3:2** Za 147:19; Mdo 7:38
[b]**3:3** Rum 10:16; Ebr 4:2; 2Tim 2:13
[c]**3:4** Yn 3:33; Za 116:11
[d]**3:5** Rum 6:19; Gal 3:15
[e]**3:6** Mwa 18:25; Rum 2:16
[f]**3:7** Rum 3:4; 9:19
[g]**3:8** Rum 6:1; Mdo 5:20; 6:1; 15
[h]**3:9** 1Fal 8:46; Gal 3:22
[i]**3:10** Za 14:1, 3; 53:1
[j]**3:12** Za 53:1-3; Mhu 7:20
[k]**3:13** Za 5:9; 140:3
[l]**3:14** Za 10:7
[m]**3:15** Isa 59:7, 8; Mit 1:16
[n]**3:17** Isa 59:7, 9
[o]**3:18** Za 36:1
[p]**3:19** Yn 10:34; Rum 2:12
[q]**3:20** Mdo 13:39; Gal 2:16; Rum 4:15; 7:7
[r]**3:21** Isa 46:13; Rum 9:30; Mdo 10:43; Rum 1:2
[s]**3:22** Rum 9:30; Gal 3:28; Kol 3:11
[t]**3:23** Rum 9:19; 5:2; 3:9; Gal 3:22
[u]**3:24** 2Kor 12:9; Tit 2:11; Za 130:7; Gal 4:5

ukombozi ulio katika Kristo Yesu. [25] [a]Yeye
ambaye Mungu alimtoa awe dhabihu ya
upatanisho kwa njia ya imani katika damu
yake. Alifanya hivi ili kuonyesha haki
yake, kwa sababu kwa ustahimili wake
aliziachilia zile dhambi zilizotangulia
kufanywa. [26] Alifanya hivyo ili kuonyesha
haki yake wakati huu, ili yeye awe mwenye
haki na mwenye kumhesabia haki yule
anayemwamini Yesu.

### *Umuhimu Wa Kuwa Na Imani*

[27] [b]Basi, kujivuna kuko wapi? Kumewekwa
mbali. Kwa sheria gani? Je, ni kwa ile ya
matendo? La hasha, bali kwa ile sheria
ya imani. [28] [c]Kwa maana twaona kwamba
mwanadamu huhesabiwa haki kwa njia ya
imani wala si kwa matendo ya sheria. [29] [d]Je,
Mungu ni Mungu wa Wayahudi peke yao?
Je, yeye si Mungu wa watu wa Mataifa pia?
Naam, yeye ni Mungu wa watu wa Mataifa
pia. [30] [e]Basi kwa kuwa tuna Mungu mmoja
tu, atawahesabia haki wale waliotahiriwa
kwa imani na wale wasiotahiriwa kwa
imani iyo hiyo. [31] Je, basi ni kwamba
tunaibatilisha sheria kwa imani hii? La,
hasha! Badala yake tunaithibitisha sheria.

### *Abrahamu Alihesabiwa Haki Kwa Imani*

4 [f]Tuseme nini basi, kuhusu Abrahamu
baba yetu kwa jinsi ya mwili: yeye
alipataje kujua jambo hili? [2] [g]Kwa maana
ikiwa Abrahamu alihesabiwa haki kwa
matendo, basi, anacho kitu cha kujivunia,
lakini si mbele za Mungu. [3] [h]Kwa maana
Maandiko yasemaje? "Abrahamu
alimwamini Mungu na ikahesabiwa kwake
kuwa haki."

[4] [i]Basi mtu afanyapo kazi, mshahara
wake hauhesabiwi kwake kuwa ni zawadi,
bali ni haki yake anayostahili. [5] [j]Lakini kwa
mtu ambaye hafanyi kazi na anamtumaini
Mungu, yeye ambaye huwahesabia waovu
haki, imani yake inahesabiwa kuwa haki.
[6] [k]Daudi pia alisema vivyo hivyo aliponena
juu ya baraka za mtu ambaye Mungu
humhesabia haki pasipo matendo:

[7] [l]"Wamebarikiwa wale
ambao wamesamehewa makosa
yao,
ambao dhambi zao zimefunikwa.
[8] [m]Heri mtu yule
Bwana hamhesabii dhambi zake."

### *Haki Kabla Ya Tohara*

[9] [n]Je, huku kubarikiwa ni kwa wale
waliotahiriwa peke yao, au pia na kwa
wale wasiotahiriwa? Tunasema, "Imani ya
Abrahamu ilihesabiwa kwake kuwa haki."
[10] [o]Je, ni lini basi ilipohesabiwa kwake
kuwa haki? Je, ilikuwa kabla au baada ya
kutahiriwa kwake? Haikuwa baada, ila kabla
hajatahiriwa. [11] [p]Alipewa ishara ya tohara
kuwa muhuri wa haki aliyokuwa nayo kwa
imani hata alipokuwa bado hajatahiriwa.
Kusudi lilikuwa kumfanya baba wa wote
wale waaminio pasipo kutahiriwa na
ambao wamehesabiwa haki. [12] [q]Vivyo
hivyo awe baba wa wale waliotahiriwa
ambao si kwamba wametahiriwa tu, bali
pia wanafuata mfano wa imani ambayo
Baba yetu Abrahamu alikuwa nayo kabla
ya kutahiriwa.

### *Ahadi Ya Mungu Hufahamika Kwa Imani*

[13] [r]Kwa maana ile ahadi kwamba
angeurithi ulimwengu haikuja kwa
Abrahamu au kwa wazao wake kwa njia
ya sheria bali kwa njia ya haki ipatikanayo
kwa imani. [14] [s]Kwa maana ikiwa wale

---

[a]**3:25** Za 65:3; Ebr 9:28; 1Pet 1:19; Ufu 1:5; Mdo 14:16; 17:30
[b]**3:27** 1Kor 1:29-31; Efe 2:9
[c]**3:28** Gal 3:11; Yn 2:19
[d]**3:29** Mdo 10:34, 35
[e]**3:30** Rum 4:11, 12; Gal 3:8
[f]**4:1** Rum 8:31; Lk 3:8
[g]**4:2** 1Kor 13:1; Mdo 13:20; 27:28
[h]**4:3** Mwa 15:6; Yak 2:23
[i]**4:4** Rum 11:6
[j]**4:5** Yos 24:2
[k]**4:6** Za 32:1, 2
[l]**4:7** Za 32:1, 2
[m]**4:8** Za 103:12; 2Kor 5:19
[n]**4:9** Rum 3:30
[o]**4:10** Rum 8:7
[p]**4:11** Mwa 17:10, 11; Lk 3:8; 19:9; Rum 3:22
[q]**4:12** Mwa 2:17; 3:19; Rum 6:23
[r]**4:13** Mdo 13:32; Gal 3:16, 29; Mwa 17:4-6
[s]**4:14** Gal 3:18

waishio kwa sheria ndio warithi, imani
haina thamani na ahadi haifai kitu, [15] [a]kwa
sababu sheria huleta ghadhabu. Mahali
ambapo hakuna sheria hakuna makosa.
[16] [b]Kwa hiyo, ahadi huja kwa njia ya
imani, ili iwe ni kwa neema, na itolewe
kwa wazao wa Abrahamu, si kwa wale
walio wa sheria peke yao, bali pia kwa wale
walio wa imani ya Abrahamu. Yeye ndiye
baba yetu sisi sote. [17] [c]Kama ilivyoandikwa:
“Nimekufanya wewe kuwa baba wa mataifa
mengi.” Yeye ni baba yetu mbele za Mungu,
ambaye yeye alimwamini, yule Mungu
anaye fufua waliokufa, na kuvitaja vile vitu
ambavyo haviko kana kwamba vimekwisha
kuwako.

*Mfano Wa Imani Ya Abrahamu*

[18] [d]Akitarajia yasiyoweza kutarajiwa,
Abrahamu akaamini, akawa baba wa
mataifa mengi, kama alivyoahidiwa
kwamba, “Uzao wako utakuwa mwingi
mno.” [19] [e]Abrahamu hakuwa dhaifu katika
imani hata alipofikiri juu ya mwili wake,
ambao ulikuwa kama uliokufa, kwani
umri wake ulikuwa unakaribia miaka mia
moja, au alipofikiri juu ya ufu wa tumbo
la Sara. [20] [f]Lakini Abrahamu hakusitasita
kwa kutokuamini ahadi ya Mungu, bali
alitiwa nguvu katika imani yake na kumpa
Mungu utukufu, [21] [g]akiwa na hakika
kabisa kwamba Mungu alikuwa na uwezo
wa kutimiza lile aliloahidi. [22] [h]Hii ndio
sababu, “ilihesabiwa kwake kuwa haki.”
[23] [i]Maneno haya “ilihesabiwa kwake kuwa
haki,” hayakuandikwa kwa ajili yake peke
yake, [24] [j]bali kwa ajili yetu sisi pia ambao
Mungu atatupa haki, sisi tunaomwamini
yeye aliyemfufua Yesu Bwana wetu kutoka
kwa wafu. [25] [k]Alitolewa afe kwa ajili ya
dhambi zetu, naye alifufuliwa kutoka mauti
ili tuhesabiwe haki.

*Matokeo Ya Kuhesabiwa Haki*

5 [l]Kwa hiyo, kwa kuwa tumekwisha
kuhesabiwa haki kwa imani, tuna
amani na Mungu kwa njia ya Bwana wetu
Yesu Kristo, [2] [m]ambaye kwa kupitia kwake
tumepata kwa njia ya imani kuifikia neema
hii ambayo ndani yake sasa tunasimama,
nasi twafurahia katika tumaini letu la
kushiriki utukufu wa Mungu. [3] [n]Si hivyo
tu, bali twafurahi pia katika mateso, kwa
sababu tunajua kuwa mateso huleta saburi,
[4] [o]nayo saburi huleta uthabiti wa moyo, na
uthabiti wa moyo huleta tumaini, [5] [p]wala
tumaini halitukatishi tamaa, kwa sababu
Mungu amekwisha kumimina pendo lake
mioyoni mwetu kwa njia ya Roho Mtakatifu
ambaye ametupatia.
[6] [q]Kwa maana hata tulipokuwa dhaifu,
wakati ulipowadia, Kristo alikufa kwa
ajili yetu sisi wenye dhambi. [7] Hakika,
ni vigumu mtu yeyote kufa kwa ajili ya
mwenye haki, ingawa inawezekana mtu
akathubutu kufa kwa ajili ya mtu mwema.
[8] [r]Lakini Mungu anaudhihirisha upendo
wake kwetu kwamba: Tulipokuwa tungali
wenye dhambi, Kristo alikufa kwa ajili yetu.
[9] [s]Basi, kwa kuwa sasa tumehesabiwa haki
kwa damu yake, si zaidi sana tutaokolewa
kutoka ghadhabu ya Mungu kupitia
kwake! [10] [t]Kwa kuwa kama tulipokuwa
adui wa Mungu tulipatanishwa naye kwa
njia ya kifo cha Mwanawe, si zaidi sana

[a]**4:15** 2Kor 3:7
[b]**4:16** Rum 3:24; 15:8
[c]**4:17** Mwa 17:5; Yn 5:21; Isa 48:13; 1Kor 1:28
[d]**4:18** Mwa 15:5
[e]**4:19** Ebr 11:11, 12; Mwa 17:17; 18:11; Mt 9:8
[f]**4:20** 1Sam 30:6; Mt 9:8; Rum 4:15; Gal 3:19
[g]**4:21** Mwa 18:14; Ebr 11:9
[h]**4:22** Rum 1:17; 9:30; Gal 2:16; 3:22
[i]**4:23** Rum 3:9; Mdo 15; 4; 1Kor 10:6, 11
[j]**4:24** Hab 2:2; 1Kor 10:11; Rum 10:9; 1Pet 1:21; Mdo 2:24
[k]**4:25** Isa 53:5, 6; 2Kor 5:21
[l]**5:1** Rum 3:28; Isa 32:17; Yn 16:33
[m]**5:2** Efe 2:18; 3:12; 1Kor 15:1; Ebr 3:5; Mt 5:12
[n]**5:3** Ebr 10:36; Yak 1:2-3; Ebr 3:6; 1Yn 3:2-3; Mdo 10:43
[o]**5:4** Yak 1:12
[p]**5:5** Flp 1:20; Ebr 3:6; Yn 3:2, 3; Rum 5:8; Yn 3:16; Rum 8:39; Tit 3:3, 6
[q]**5:6** Mk 1:15; Efe 1:10; Rum 4:25
[r]**5:8** Yn 3:16; 1Yn 4:10
[s]**5:9** Rum 3:25; Kum 1:18
[t]**5:10** Rum 11:28; 1Kor 1:21; 2Kor 5:18, 19; Kol 1:20, 22; Ebr 7:25

tukiisha kupatanishwa, tutaokolewa kwa
uzima wake. 11 [a]Lakini zaidi ya hayo, pia
tunafurahi katika Mungu kwa njia ya
Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kupitia
kwake tumepata upatanisho.

### *Adamu Alileta Kifo, Yesu Ameleta Uzima*

12 [b]Kwa hiyo kama vile dhambi ilivyoingia
ulimwenguni kupitia kwa mtu mmoja, na
kupitia dhambi hii mauti ikawafikia watu
wote, kwa sababu wote wamefanya dhambi:
13 [c]kwa maana kabla sheria haijatolewa,
dhambi ilikuwepo ulimwenguni. Lakini
dhambi haihesabiwi wakati hakuna sheria.
14 [d]Hata hivyo, tangu wakati wa Adamu hadi
wakati wa Mose, mauti ilitawala watu wote,
hata wale ambao hawakutenda dhambi
kwa kuvunja amri, kama alivyofanya
Adamu, ambaye alikuwa mfano wa yule
atakayekuja.

15 [e]Lakini ile karama iliyotolewa haikuwa
kama lile kosa. Kwa maana ikiwa watu
wengi walikufa kwa sababu ya kosa la
mtu mmoja, zaidi sana neema ya Mungu
na ile karama iliyokuja kwa neema ya
mtu mmoja, yaani, Yesu Kristo, imezidi
kuwa nyingi kwa ajili ya wengi. 16 Tena,
ile karama ya Mungu si kama matokeo ya
ile dhambi. Hukumu ilikuja kwa njia ya
mtu mmoja, ikaleta adhabu, bali karama
ya neema ya Mungu ilikuja kwa njia ya
makosa mengi, ikaleta kuhesabiwa haki.
17 Kwa maana ikiwa kutokana na kosa la
mtu mmoja, mauti ilitawala kupitia huyo
mtu mmoja, zaidi sana wale wanaopokea
wingi wa neema ya Mungu na karama yake
ya kuhesabiwa haki, watatawala katika
uzima kwa njia ya huyo mtu mmoja, yaani,
Yesu Kristo.

18 [f]Kwa hiyo, kama vile kosa la mtu
mmoja lilivyoleta adhabu kwa watu wote,
vivyo hivyo pia kwa tendo la haki la mtu
mmoja lilileta kuhesabiwa haki ambako
huleta uzima kwa wote. 19 [g]Kwa maana
kama vile kwa kutokutii kwa yule mtu
mmoja wengi walifanywa wenye dhambi,
vivyo hivyo kwa kutii kwa mtu mmoja
wengi watafanywa wenye haki.

20 [h]Zaidi ya hayo, sheria ilikuja, ili
uvunjaji wa sheria uongezeke. Lakini
dhambi ilipoongezeka, neema iliongezeka
zaidi, 21 [i]ili kwamba kama vile dhambi
ilivyotawala kwa njia ya mauti, vivyo
hivyo neema iweze kutawala kwa njia ya
kuhesabiwa haki hata kuleta uzima wa
milele katika Yesu Kristo Bwana wetu.

### *Kufa Na Kufufuka Pamoja Na Kristo*

6 [j]Tuseme nini basi? Je, tuendelee kutenda
dhambi ili neema ipate kuongezeka? 2 [k]La
hasha! Sisi tulioifia dhambi, tutawezaje
kuendelea kuishi tena katika dhambi? 3 [l]Au
hamjui ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika
Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake?
4 [m]Kwa hiyo tulizikwa pamoja naye kwa
njia ya ubatizo katika mauti, ili kama vile
Kristo alivyofufuliwa kutoka kwa wafu kwa
utukufu wa Baba, vivyo hivyo sisi nasi pia
tupate kuenenda katika upya wa uzima.

5 [n]Kwa maana ikiwa tumeungana
naye katika mauti yake, bila shaka
tutaungana naye katika ufufuo wake.
6 [o]Kwa maana twajua kwamba utu wetu
wa kale ulisulubiwa pamoja naye ili ule
mwili wa dhambi upate kuangamizwa,
nasi tusiendelee kuwa tena watumwa wa
dhambi. 7 [p]Kwa maana mtu yeyote aliyekufa
amehesabiwa haki mbali na dhambi.

8 [q]Basi ikiwa tulikufa pamoja na Kristo,
tunaamini kwamba pia tutaishi pamoja

---

[a]**5:11** Rum 5:10; 2:17; 3:29, 30; Gal 4:9
[b]**5:12** Mwa 3:1-7; 1Kor 15:21, 22; Mwa 3:19; Rum 6:23
[c]**5:13** Rum 4:15
[d]**5:14** 1Kor 15:22, 45
[e]**5:15** Mdo 15:11
[f]**5:18** Rum 4:25
[g]**5:19** Flp 2:8
[h]**5:20** Rum 3:20; Gal 3:19; Rum 6:1; 1Tim 1:13, 14
[i]**5:21** Rum 6:16
[j]**6:1** Rum 3:5, 6
[k]**6:2** Kol 3:5, 8
[l]**6:3** Mt 28:19
[m]**6:4** Mdo 2:24; Kol 2:12; 2Kor 5:17; Gal 6:15
[n]**6:5** Efe 2:6; 2Tim 2:11
[o]**6:6** Gal 5:24; Kol 3:9; 2Kor 4:10; Gal 2:20; Rum 7:24
[p]**6:7** 1Pet 4:1; Rum 6:18
[q]**6:8** Rum 6:5; 2Tim 2:11

naye. 9 [a]Kwa maana tunajua kwamba
Kristo, kwa sababu alifufuliwa kutoka
kwa wafu, hawezi kufa tena; mauti haina
tena mamlaka juu yake. 10 [b]Kifo alichokufa,
aliifia dhambi mara moja tu, lakini uzima
alio nao anamwishia Mungu.

11 [c]Vivyo hivyo, jihesabuni wafu katika
dhambi lakini mlio hai kwa Mungu katika
Kristo Yesu. 12 [d]Kwa hiyo, msiruhusu dhambi
itawale ndani ya miili yenu, ipatikanayo na
kufa, ili kuwafanya mzitii tamaa mbaya.
13 [ef]Wala msivitoe viungo vya miili yenu
vitumike kama vyombo vya uovu vya
kutenda dhambi, bali jitoeni kwa Mungu,
kama watu waliotolewa kutoka mautini
kuingia uzimani. Nanyi vitoeni viungo
vya miili yenu kwake kama vyombo vya
haki. 14 [g]Kwa maana dhambi haitakuwa
na mamlaka juu yenu, kwa sababu hampo
chini ya sheria, bali chini ya neema.

*Watumwa Wa Haki*

15 [h]Ni nini basi? Je, tutende dhambi
kwa kuwa hatuko chini ya sheria bali
chini ya neema? La, hasha! 16 [i]Je, hamjui
kwamba mnapojitoa kwa mtu yeyote kama
watumwa watiifu, ninyi ni watumwa wa
yule mnayemtii, aidha watumwa wa
dhambi, ambayo matokeo yake ni mauti,
au watumwa wa utii ambao matokeo yake
ni haki? 17 [j]Lakini Mungu ashukuriwe
kwa kuwa ninyi ambao kwanza mlikuwa
watumwa wa dhambi, mmekuwa watii
kutoka moyoni kwa mafundisho mliyopewa.
18 [k]Nanyi, mkiisha kuwekwa huru mbali na
dhambi, mmekuwa watumwa wa haki.

19 [l]Ninasema kwa namna ya kibinadamu
kwa sababu ya udhaifu wenu wa hali ya asili.
Kama vile mlivyokuwa mkivitoa viungo
vya miili yenu kama watumwa wa mambo
machafu na uovu uliokuwa ukiongezeka
zaidi, hivyo sasa vitoeni viungo vyenu
kama watumwa wa haki inayowaelekeza
mpate kutakaswa. 20 [m]Mlipokuwa watumwa
wa dhambi, mlikuwa hamtawaliwi na
haki. 21 [n]Lakini mlipata faida gani kwa
mambo hayo ambayo sasa mnayaonea
aibu? Mwisho wa mambo hayo ni mauti.
22 [o]Lakini sasa kwa kuwa mmewekwa huru
mbali na dhambi na mmekuwa watumwa
wa Mungu, faida mnayopata ni utakatifu,
ambao mwisho wake ni uzima wa milele.
23 [p]Kwa maana mshahara wa dhambi ni
mauti, bali karama ya Mungu ni uzima wa
milele katika Kristo Yesu Bwana wetu.

*Hatufungwi Tena Na Sheria*

7 [q]Ndugu zangu (sasa ninasema na wale
wanaoijua sheria), je, hamjui ya kwamba
sheria ina mamlaka tu juu ya mtu wakati
akiwa hai? 2 [r]Kwa mfano, mwanamke
aliyeolewa amefungwa kwa mumewe
wakati akiwa hai, lakini yule mume akifa,
yule mwanamke amefunguliwa kutoka
sheria ya ndoa. 3 [s]Hivyo basi, kama huyo
mwanamke ataolewa na mwanaume
mwingine wakati mumewe akiwa bado
yuko hai, ataitwa mzinzi. Lakini kama
mumewe akifa, mwanamke huyo hafungwi
tena na sheria ya ndoa, naye akiolewa na
mtu mwingine haitwi mzinzi.

4 [t]Vivyo hivyo, ndugu zangu, ninyi
mmeifia sheria kwa njia ya mwili wa Kristo,
ili mweze kuwa mali ya mwingine, yeye
ambaye alifufuliwa kutoka kwa wafu, ili
tupate kuzaa matunda kwa Mungu. 5 [u]Kwa
maana tulipokuwa tunatawaliwa na asili ya
dhambi, tamaa za dhambi zilizochochewa
na sheria zilikuwa zikitenda kazi katika

[a]**6:9** Mdo 2:24; Ufu 1:18
[b]**6:10** Rum 6:2; Ebr 7:27; 9:26-28; Gal 2:19; 1Pet 3:18
[c]**6:11** Rum 6:2; 2Kor 5:15; 1Pet 2:24
[d]**6:12** Rum 6:16; Mwa 4:7; Za 19:13; 119:133
[e]**6:13** Rum 7:5; 2Kor 5:15
[f]**6:13** 1Pet 2:24
[g]**6:14** Rum 2:12; Gal 5:18; Rum 3:24
[h]**6:15** 1Kor 9:21
[i]**6:16** Za 51:5; 2Pet 2:19
[j]**6:17** Rum 1:18; 2Kor 2:14; 2Tim 1:13
[k]**6:18** Rum 8:2; 1Pet 4:1
[l]**6:19** Rum 3:5; Gal 3:15
[m]**6:20** Rum 6:16; Yn 8:34
[n]**6:21** Rum 6:23; Eze 16:61, 63; Rum 8:6, 13
[o]**6:22** 1Pet 2:16
[p]**6:23** Mit 10:16; Yak 1:15; Mt 25:46
[q]**7:1** Gal 3:15; 5:18
[r]**7:2** 1Kor 7:39
[s]**7:3** Lk 16:18; Mt 5:32
[t]**7:4** Gal 2:19; 4:31; Kol 1:22
[u]**7:5** Rum 7:7-11; 6:13

miili yetu, hivyo tulizaa matunda ya mauti.
6 [a]Lakini sasa, kwa kufia kile kilichokuwa
kimetufunga kwanza, tumewekwa huru
kutokana na sheria ili tutumike katika
njia mpya ya Roho, wala si katika njia ya
zamani ya sheria iliyoandikwa.

*Sheria Na Dhambi*

7 [b]Tuseme nini basi? Kwamba sheria ni
dhambi? La, hasha! Lakini, isingekuwa
kwa sababu ya sheria, nisingalijua dhambi.
Nisingalijua kutamani ni nini kama sheria
haikusema, "Usitamani." 8 [c]Lakini dhambi
kwa kupata nafasi katika amri, hii ikazaa
ndani yangu kila aina ya tamaa. Kwa
maana pasipo sheria, dhambi imekufa.
9 Wakati fulani nilikuwa hai pasipo sheria,
lakini amri ilipokuja, dhambi ikawa hai,
nami nikafa. 10 [d]Nikaona kwamba ile amri
iliyokusudiwa kuleta uzima, ilileta mauti.
11 [e]Kwa maana dhambi kwa kupata nafasi
katika amri, ilinidanganya, na kupitia
katika hiyo amri, ikaniua. 12 [f]Hivyo basi,
sheria yenyewe ni takatifu, na amri ni
takatifu na ya haki, tena ni njema.

13 [g]Je, kile kilicho chema basi kilikuwa
mauti kwangu? La, hasha! Lakini ili dhambi
itambuliwe kuwa ni dhambi, ilileta mauti
ndani yangu kupitia kile kilichokuwa
chema, ili kwa njia ya amri dhambi izidi
kuwa mbaya kupita kiasi.

*Mgongano Wa Ndani*

14 [h]Kwa maana tunajua kwamba sheria
ni ya kiroho, lakini mimi ni wa kimwili
nikiwa nimeuzwa kwenye utumwa wa
dhambi. 15 [i]Sielewi nitendalo, kwa maana
lile ninalotaka kulitenda, silitendi, lakini
ninatenda lile ninalolichukia. 16 [j]Basi
kama ninatenda lile nisilotaka kutenda, ni
kwamba ninakubali kuwa sheria ni njema.
17 [k]Lakini, kwa kweli si mimi tena nitendaye
lile nisilotaka bali ni ile dhambi ikaayo
ndani yangu. 18 [l]Kwa maana ninafahamu
kwamba hakuna jema lolote likaalo ndani
yangu, yaani, katika asili yangu ya dhambi.
Kwa kuwa nina shauku ya kutenda lililo
jema, lakini siwezi kulitenda. 19 [m]Sitendi
lile jema nitakalo kutenda, bali lile baya
nisilolitaka, ndilo nitendalo. 20 [n]Basi kama
ninatenda lile nisilotaka kutenda, si mimi
tena nifanyaye hivyo, bali ni ile dhambi
ikaayo ndani yangu.

21 [o]Hivyo naiona sheria ikitenda kazi.
Ninapotaka kutenda jema, jambo baya liko
papo hapo. 22 [p]Kwa maana katika utu wangu
wa ndani naifurahia sheria ya Mungu.
23 [q]Lakini ninaona kuna sheria nyingine
inayotenda kazi katika viungo vya mwili
wangu inayopigana vita dhidi ya ile sheria
ya akili yangu. Sheria hii inanifanya mateka
wa ile sheria ya dhambi inayofanya kazi
katika viungo vya mwili wangu.

24 [r]Ole wangu mimi maskini! Ni nani
atakayeniokoa na mwili huu wa mauti?

25 Ashukuriwe Mungu kwa njia ya Yesu
Kristo Bwana wetu! Hivyo basi, mimi
mwenyewe kwa akili zangu ni mtumwa
wa sheria ya Mungu, lakini katika asili ya
dhambi ni mtumwa wa sheria ya dhambi.

*Maisha Katika Roho*

8 [s]Kwa hiyo, sasa hakuna hukumu ya
adhabu kwa wale walio ndani ya
Kristo Yesu, wale ambao hawaenendi kwa
kuufuata mwili bali kwa kufuata Roho.
2 [t]Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima
katika Kristo Yesu imeniweka huru mbali na
sheria ya dhambi na mauti. 3 [u]Kwa maana

[a]**7:6** Rum 2:29
[b]**7:7** Rum 3:20; 4:15; Kut 20:17; Kum 5:21
[c]**7:8** Rum 4:15; 1Kor 15:56
[d]**7:10** Law 18:5; Lk 10:26-28
[e]**7:11** Mwa 3:13
[f]**7:12** Gal 3:21; 1Tim 1:8
[g]**7:13** Rum 6:23; 7:12; 5:20
[h]**7:14** 1Kor 3:1; 1Fal 21:20-25; 2Fal 17:17
[i]**7:15** Gal 5:17
[j]**7:16** Rum 7:12
[k]**7:17** Rum 7:20
[l]**7:18** Gal 5:24
[m]**7:19** Rum 7:15
[n]**7:20** Rum 7:17
[o]**7:21** Rum 7:23, 25
[p]**7:22** Efe 3:16; Za 1:2; 40:8
[q]**7:23** Yak 4:1; 1Pet 2:11
[r]**7:24** Rum 6:6; 8:2
[s]**8:1** Rum 16:3; 8:34, 39; 16:3
[t]**8:2** 1Kor 15:45; Rum 6:18; 6:16; 7:4
[u]**8:3** Mdo 13:39; Ebr 10:1-4; 2:14, 17

kile ambacho sheria haikuwa na uwezo wa
kufanya, kwa vile ilivyokuwa dhaifu katika
mwili, Mungu kwa kumtuma Mwanawe
mwenyewe kwa mfano wa mwanadamu
mwenye mwili ulio wa dhambi na kwa ajili
ya dhambi, yeye aliihukumu dhambi katika
mwili, 4 [a]ili kwamba haki ipatikanayo kwa
sheria itimizwe ndani yetu sisi, ambao
hatuenendi kwa kuufuata mwili bali kwa
kufuata Roho.

5 [b]Kwa maana wale wanaoishi kwa
kuufuata mwili huziweka nia zao katika
vitu vya mwili, lakini wale wanaoishi kwa
kufuata Roho, huziweka nia zao katika
mambo ya Roho. 6 [c]Kwa maana kuwa na
nia ya mwili ni mauti, bali kuwa na nia
inayoongozwa na Roho ni uzima na amani.
7 [d]Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui na
Mungu, kwa maana haiitii sheria ya Mungu,
wala haiwezi kuitii. 8 [e]Wale wanaotawaliwa
na mwili, hawawezi kumpendeza Mungu.

9 [f]Lakini ninyi, hamtawaliwi na mwili,
bali na Roho, ikiwa Roho wa Mungu anakaa
ndani yenu. Mtu yeyote ambaye hana Roho
wa Kristo, yeye si wa Kristo. 10 [g]Lakini
kama Kristo anakaa ndani yenu, miili yenu
imekufa kwa sababu ya dhambi, lakini roho
zenu zi hai kwa sababu ya haki. 11 [h]Nanyi
ikiwa Roho wa Mungu aliyemfufua Yesu
kutoka kwa wafu anakaa ndani yenu, yeye
aliyemfufua Kristo Yesu kutoka kwa wafu
ataihuisha pia miili yenu ambayo hufa, kwa
njia ya Roho wake akaaye ndani yenu.

12 [i]Kwa hiyo ndugu zangu, sisi tu wadeni,
si wa mwili, ili tuishi kwa kuufuata mwili,
13 [j]kwa maana mkiishi kwa kuufuata mwili,
mtakufa, lakini kama mkiyaua matendo
ya mwili kwa Roho, mtaishi. 14 [k]Kwa kuwa
wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu,
hao ndio watoto wa Mungu. 15 [l]Kwa
maana hamkupokea roho ya utumwa
iwaleteayo tena hofu, bali mlipokea roho ya
kufanywa wana, ambaye kwa yeye twalia,
"Abba,[m] yaani, Baba," 16 [n]Roho mwenyewe
hushuhudia pamoja na roho zetu ya
kwamba sisi tu watoto wa Mungu. 17 [o]Hivyo,
ikiwa sisi ni watoto, basi tu warithi, warithi
wa Mungu, warithio pamoja na Kristo,
naam, tukiteswa pamoja naye tupate pia
kutukuzwa pamoja naye.

*Utukufu Ujao*

18 [p]Nayahesabu mateso yetu ya wakati
huu kuwa si kitu kulinganisha na utukufu
utakaodhihirishwa kwetu. 19 [q]Kwa maana
viumbe vyote vinangoja kwa shauku
kudhihirishwa kwa watoto wa Mungu.
20 [r]Kwa kuwa viumbe vyote viliwekwa
chini ya ubatili, si kwa chaguo lao, bali
kwa mapenzi yake yeye aliyevitiisha katika
tumaini, 21 [s]ili kwamba viumbe vyote vipate
kuwekwa huru kutoka kwa utumwa wa
kuharibika na kupewa uhuru wa utukufu
wa watoto wa Mungu.

22 [t]Kwa maana twajua ya kuwa hata
sasa viumbe vyote vimekuwa vikilia kwa
maumivu kama utungu wa mwanamke
wakati wa kuzaa. 23 [u]Wala si hivyo viumbe
peke yao, bali hata sisi ambao ndio matunda
ya kwanza ya Roho, kwa ndani tunalia kwa
uchungu tukisubiri kwa shauku kufanywa
wana wa Mungu, yaani, ukombozi wa miili
yetu. 24 [v]Kwa kuwa tuliokolewa kwa tumaini
hili. Lakini kama kinachotumainiwa
kikionekana hakiwi tumaini tena. Je, kuna
mtu anayetumaini kupata kitu alicho nacho

---

[a]**8:4** Rum 2:26; Gal 5:16, 25
[b]**8:5** Gal 5:19-21
[c]**8:6** Rum 6:21, 23; 8:13; Gal 6:8
[d]**8:7** Yak 4:4; Mt 12:34; Yn 8:43; 12:39
[e]**8:8** Gal 5:24
[f]**8:9** Kol 4:6; 2Tim 1:14; Mdo 16:7; 1Yn 4:13
[g]**8:10** Kol 1:27; Ufu 3:20
[h]**8:11** Mdo 2:24; Yn 5:21; Rum 6:5
[i]**8:12** Rum 6:7, 18
[j]**8:13** Gal 6:8; Rum 6:23; 6; 2; 8:6; Gal 6:8
[k]**8:14** Gal 5:18; Hes 1:10; Efe 1:5
[l]**8:15** 2Tim 1:7; Ebr 2:15; Mk 14:36; Kol 4:5, 6
[m]15 Abba ni neno la Kiaramu ambalo maana yake ni Baba; ni neno ambalo lingetumiwa na mtoto kwa yule ambaye amemzaa.
[n]**8:16** 2Kor 1:22; Efe 1:13
[o]**8:17** Efe 3:6; Tit 3:7; 2Tim 2:12; 1Pet 4:13
[p]**8:18** 1Pet 4:13
[q]**8:19** Rum 8:14
[r]**8:20** Mwa 3:17-19; 5:29
[s]**8:21** 2Pet 3:13; Ufu 21:1
[t]**8:22** Yer 12:4
[u]**8:23** 2Kor 5:5; 5:2, 4; Gal 5:5
[v]**8:24** 1The 5:8; Tit 3:7

tayari? 25 [a]Lakini tunapotumaini kupata kitu
ambacho hatuna, basi twakingojea kwa
saburi.
26 [b]Vivyo hivyo, Roho hutusaidia
katika udhaifu wetu, kwa sababu hatujui
kuomba ipasavyo. Lakini Roho mwenyewe
hutuombea kwa uchungu usioweza
kutamkwa. 27 [c]Naye Mungu aichunguzaye
mioyo, anaijua nia ya Roho, kwa sababu
Roho huwaombea watakatifu sawasawa na
mapenzi ya Mungu.

### *Tunashinda Na Zaidi Ya Kushinda*

28 [d]Nasi tunajua ya kuwa katika mambo
yote Mungu hutenda kazi pamoja na wote
wampendao, katika kuwapatia mema,
yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake.
29 [e]Maana wale Mungu aliowajua tangu
mwanzo, pia aliwachagua tangu mwanzo,
wapate kufanana na mfano wa Mwanawe,
ili yeye awe mzaliwa wa kwanza miongoni
mwa ndugu wengi. 30 [f]Nao wale Mungu
aliotangulia kuwachagua, akawaita, wale
aliowaita pia akawahesabia haki, nao wale
aliowahesabia haki, pia akawatukuza.

### *Upendo Wa Mungu*

31 [g]Tuseme nini basi kuhusu haya?
Ikiwa Mungu yuko upande wetu, ni nani
awezaye kuwa kinyume chetu? 32 [h]Ikiwa
Mungu hakumhurumia Mwanawe, bali
alimtoa kwa ajili yetu sote, atakosaje basi
kutupatia vitu vyote kwa ukarimu pamoja
naye? 33 [i]Ni nani atakayewashtaki wale
ambao Mungu amewateua? Ni Mungu
mwenyewe ndiye mwenye kuwahesabia
haki. 34 [j]Ni nani basi atakayewahukumia
adhabu? Kristo Yesu aliyekufa, naam, zaidi
ya hayo, aliyefufuliwa kutoka kwa wafu,
yuko mkono wa kuume wa Mungu, naye
pia anatuombea. 35 [k]Ni nani atakayetutenga
na upendo wa Kristo? Je, ni shida au taabu
au mateso au njaa au uchi au hatari au
upanga? 36 [l]Kama ilivyoandikwa:

"Kwa ajili yako tunauawa mchana
kutwa;
tumehesabiwa kama kondoo wa
kuchinjwa."

37 [m]Lakini katika mambo haya yote
tunashinda, naam na zaidi ya kushinda,
kwa yeye aliyetupenda. 38 [n]Kwa maana
nimekwisha kujua kwa hakika ya kuwa
sio mauti, wala uzima, wala malaika,
wala wenye mamlaka, wala yaliyopo, wala
yatakayokuja, wala wenye uwezo, 39 [o]wala
yaliyo juu, wala yaliyo chini, wala kiumbe
kingine chochote zitaweza kututenga na
upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu,
Bwana wetu.

### *Kuteuliwa Kwa Israeli Na Mungu*

9 [p]Ninasema kweli katika Kristo,
wala sisemi uongo, dhamiri yangu
inanishuhudia katika Roho Mtakatifu.
2 [q]Nina huzuni kuu na uchungu usiokoma
moyoni mwangu. 3 [r]Kwa maana ningetamani
hata mimi nilaaniwe na kutengwa na Kristo
kwa ajili ya ndugu zangu hasa, wale walio
wa kabila langu kwa jinsi ya mwili, 4 [s]yaani,
watu wa Israeli, ambao ndio wenye kule
kufanywa wana, ule utukufu wa Mungu,
yale maagano, kule kupokea sheria, ibada
ya kwenye Hekalu na zile ahadi. 5 [t]Wao ni
wa uzao wa mababa wakuu wa kwanza,
ambao kutoka kwao Kristo alikuja kwa jinsi
ya mwili kama mwanadamu, yeye ambaye

[a]**8:25** Za 37:7
[b]**8:26** Efe 6:18
[c]**8:27** Ufu 2:23
[d]**8:28** Ebr 9:15; 1Pet 2:9
[e]**8:29** Rum 11:2; 1Pet 1:2; Efe 1:5, 11; Flp 3:21; 1Yn 3:2
[f]**8:30** Efe 1:5, 11; Rum 4:25; 1Kor 6:11; Rum 9:23
[g]**8:31** Rum 6:1; 7:7; Isa 8:10; Ebr 13:6
[h]**8:32** Mt 3:17; Yn 3:16
[i]**8:33** Isa 50:8, 9
[j]**8:34** Rum 5:6-8; Mk 16:19; Ay 16:20; Yn 2:1
[k]**8:35** 1Kor 4:11; 2Kor 11:26, 27
[l]**8:36** Za 44:22; 2Kor 6:9
[m]**8:37** 1Kor 15:57; Efe 5:2; Ufu 3:9
[n]**8:38** Kol 1:16; 1Pet 3:22
[o]**8:39** Rum 5:8
[p]**9:1** Gal 1:20; 1Tim 2:7; Rum 1:9
[q]**9:2** Rum 10:1
[r]**9:3** Kut 32:32; 1Kor 12:3; 16:22; Rum 11:14
[s]**9:4** Kut 6:7; Kum 7:6; 4:13; Flp 1:12; Za 147:19; Ebr 9:1; Mdo 13:32; Gal 3:16
[t]**9:5** Mt 1:1-16; Yn 1:1; Kol 2:9; Rum 1:3, 25; 2Kor 11:31

ni Mungu aliye juu ya vyote, mwenye
kuhimidiwa milele! Amen.
[6] [a]Si kwamba Neno la Mungu
limeshindwa. Kwa maana si kila Mwisraeli
ambaye ni wa uzao utokanao na Israeli ni
Mwisraeli halisi. [7] [b]Wala hawakuwi wazao
wa Abrahamu kwa sababu wao ni watoto
wake, lakini: "Uzao wako utahesabiwa
kupitia kwake Isaki." [8] [c]Hii ina maana
kwamba, si watoto waliozaliwa kimwili
walio watoto wa Mungu, bali ni watoto
wa ahadi wanaohesabiwa kuwa uzao wa
Abrahamu. [9] [d]Kwa maana ahadi yenyewe
ilisema, "Nitakurudia tena wakati kama
huu, naye Sara atapata mtoto wa kiume."
[10] [e]Wala si hivyo tu, bali pia watoto
aliowazaa Rebeka walikuwa na baba
huyo huyo mmoja, yaani, baba yetu
Isaki. [11] [f]Lakini, hata kabla hao mapacha
hawajazaliwa au kufanya jambo lolote
jema au baya, ili kwamba kusudi la
Mungu la kuchagua lipate kusimama,
[12] [g]si kwa matendo, bali kwa yeye mwenye
kuita, Rebeka aliambiwa, "Yule mkubwa
atamtumikia yule mdogo." [13] [h]Kama vile
ilivyoandikwa, "Nimempenda Yakobo,
lakini nimemchukia Esau."

*Mungu Hana Upendeleo*

[14] [i]Tuseme nini basi? Je, Mungu ni
dhalimu? La, hasha! [15] [j]Kwa maana Mungu
alimwambia Mose,

"Nitamrehemu yeye nimrehemuye,
na pia nitamhurumia yeye
nimhurumiaye."

[16] [k]Kwa hiyo haitegemei kutaka kwa
mwanadamu au jitihada, bali hutegemea
huruma ya Mungu. [17] [l]Kwa maana Maandiko
yamwambia Farao, "Nilikuinua kwa kusudi
hili hasa, ili nipate kuonyesha uweza
wangu juu yako, na ili Jina langu lipate
kutangazwa duniani yote."
[18] [m]Kwa hiyo basi, Mungu humhurumia
yeye atakaye kumhurumia na humfanya
mgumu yeye atakaye kumfanya mgumu.
[19] [n]Basi mtaniambia, "Kama ni hivyo, kwa
nini basi bado Mungu anatulaumu? Kwa
maana ni nani awezaye kupinga mapenzi
yake?" [20] [o]Lakini, ewe mwanadamu, u
nani wewe ushindane na Mungu? "Je,
kilichoumbwa chaweza kumwambia yeye
aliyekiumba, 'Kwa nini umeniumba hivi?' "
[21] [p]Je, mfinyanzi hana haki ya kufinyanga
kutoka bonge moja vyombo vya udongo,
vingine kwa matumizi ya heshima na
vingine kwa matumizi ya kawaida?
[22] [q]Iweje basi, kama Mungu kwa kutaka
kuonyesha ghadhabu yake na kufanya
uweza wake ujulikane, amevumilia kwa
uvumilivu mwingi vile vyombo vya
ghadhabu vilivyoandaliwa kwa uharibifu?
[23] [r]Iweje basi, kama yeye alitenda hivi ili
kufanya wingi wa utukufu wake ujulikane
kwa vile vyombo vya rehema yake,
alivyotangulia kuvitengeneza kwa ajili ya
utukufu wake, [24] [s]yaani pamoja na sisi,
ambao pia alituita, si kutoka kwa Wayahudi
peke yao, bali pia kutoka kwa watu wa
Mataifa?

*Yote Yalitabiriwa Katika Maandiko*

[25] [t]Kama vile Mungu asemavyo katika
Hosea:

"Nitawaita 'watu wangu'
wale ambao si watu wangu;
nami nitamwita 'mpenzi wangu'
yeye ambaye si mpenzi wangu,"

[a]**9:6** Rum 2:28, 29; Gal 6:16
[b]**9:7** Mwa 21:12; Ebr 11:18
[c]**9:8** Rum 8:14; Gal 3:16; 4:23
[d]**9:9** Mwa 18:10; 18:14
[e]**9:10** Mwa 25:23; 25:21
[f]**9:11** Rum 8:28; 9:16; 8:28
[g]**9:12** Mwa 25:23
[h]**9:13** Mal 1:2-3; Kum 21:15; Mit 13:24; Mt 10:37; Lk 14:26; Yn 12:25
[i]**9:14** 2Nya 19:7; Kum 32:4; Ay 8:3; 34:10; Za 92:15
[j]**9:15** Kut 33:19
[k]**9:16** Efe 2:8; Tit 3:5
[l]**9:17** Kut 14:4; Za 76:10
[m]**9:18** Yos 11:20; Rum 11:25
[n]**9:19** 1Kor 15:35; Yos 2:18; 2Sam 16:10; Dan 4:35
[o]**9:20** Isa 64:8; Yer 18:6; Isa 10:15
[p]**9:21** 2Tim 2:20
[q]**9:22** Rum 2:4
[r]**9:23** Rum 8:28; 8:30
[s]**9:24** Rum 8:28; 3:29
[t]**9:25** Hos 2:23; 1Pet 2:10

26 [a]tena,

“Itakuwa hasa mahali pale
walipoambiwa,
‘Ninyi si watu wangu,’
wao wataitwa ‘wana wa Mungu aliye
hai.’ ”

27 [b]Isaya anapiga kelele kuhusu Israeli:

“Ingawa idadi ya wana wa Israeli
ni wengi kama mchanga wa
pwani,
ni mabaki yao tu watakaookolewa.
28 Kwa kuwa Bwana ataitekeleza
hukumu yake duniani kwa haraka
na kwa ukamilifu.”

29 [c]Ni kama vile alivyotabiri Isaya
akisema:

“Kama Bwana Mwenye Nguvu Zote
asingelituachia uzao,
tungelikuwa kama Sodoma,
tungelifanana na Gomora.”

*Kutokuamini Kwa Israeli*

30 [d]Kwa hiyo tuseme nini basi? Kwamba
watu wa Mataifa ambao hawakutafuta haki,
wamepata haki ile iliyo kwa njia ya imani.
31 [e]Lakini Israeli, ambao walijitahidi kupata
haki kwa njia ya sheria, hawakuipata.
32 [f]Kwa nini? Kwa sababu hawakuitafuta
kwa njia ya imani bali kwa njia ya matendo.
Wakajikwaa kwenye lile “jiwe la kukwaza.”
33 [g]Kama ilivyoandikwa:

“Tazama naweka katika Sayuni jiwe
la kukwaza watu
na mwamba wa kuwaangusha.
Yeyote atakayemwamini
hataaibika kamwe.”

10 [h]Ndugu zangu, shauku ya moyo wangu
na maombi yangu kwa Mungu ni kwa
ajili ya Waisraeli, kwamba waokolewe.
2 [i]Kwa maana ninaweza nikashuhudia wazi
kwamba wao wana juhudi kubwa kwa ajili
ya Mungu, lakini juhudi yao haina maarifa.
3 [j]Kwa kuwa hawakuijua haki itokayo
kwa Mungu, wakatafuta kuweka haki
yao wenyewe, hawakujitia chini ya haki
ya Mungu. 4 Kwa maana Kristo ni ukomo
wa sheria ili kuwe na haki kwa kila mtu
aaminiye.

*Wokovu Ni Kwa Ajili Ya Wote*

5 Mose anaandika kuhusu haki ile
itokanayo na sheria, kwamba, “Mtu
atendaye matendo hayo ataishi kwa
hayo.” 6 [k]Lakini ile haki itokanayo na
imani husema hivi: “Usiseme moyoni
mwako, ‘Ni nani atakayepanda mbinguni?’ ”
(yaani ili kumleta Kristo chini) 7 [l]“au ‘Ni
nani atashuka kwenda kuzimu?’ ” (yaani
ili kumleta Kristo kutoka kwa wafu.)
8 [m]Lakini andiko lasemaje? “Lile neno
liko karibu nawe, liko kinywani mwako
na moyoni mwako,” yaani, lile neno la
imani tunalolihubiri. 9 [n]Kwa sababu kama
ukikiri kwa kinywa chako kwamba “Yesu
ni Bwana,” na kuamini moyoni mwako
kwamba Mungu alimfufua kutoka kwa
wafu, utaokoka. 10 Kwa maana kwa moyo
mtu huamini na hivyo kuhesabiwa haki,
tena kwa kinywa mtu hukiri na hivyo
kupata wokovu. 11 [o]Kama yasemavyo
Maandiko, “Yeyote amwaminiye hataaibika
kamwe.” 12 Kwa maana hakuna tofauti kati
ya Myahudi na Myunani, yeye ni Bwana wa
wote, mwenye utajiri kwa wote wamwitao.
13 [p]Kwa maana, “Kila mtu atakayeliitia Jina
la Bwana, ataokolewa.”
14 [q]Lakini watamwitaje yeye ambaye
hawajamwamini? Nao watawezaje

[a]**9:26** Hos 1:10; Mt 16:16
[b]**9:27** Mwa 22:17; Isa 10:22-23; Hos 1:10; Yoe 2:32; Rum 11:5
[c]**9:29** Yak 5:4; Isa 1:9; 13:19; Yer 50; 40
[d]**9:30** Flp 3:9; Ebr 11:17
[e]**9:31** Isa 51:11; Rum 11:7; Gal 5:4
[f]**9:32** 1Pet 2:8
[g]**9:33** Isa 8:14; 1Pet 2:6, 8
[h]**10:1** Za 20:4; Mdo 22:23
[i]**10:2** Mdo 21:20; 22:3; Gal 1:14; 4:17; Rum 9:32
[j]**10:3** Rum 1:17; 9:31; Flp 3:9
[k]**10:6** Rum 9:30; Kut 30:12
[l]**10:7** Kum 30:13; Mdo 2:24
[m]**10:8** Kum 30:14
[n]**10:9** Mt 10:32; Lk 12:8; Mdo 2:24
[o]**10:11** Isa 28:16; Mt 28:18; Mdo 10:36
[p]**10:13** Mdo 2:21; Yoe 2:32
[q]**10:14** Tit 1:3

kumwamini yeye ambaye hawajamsikia?
Tena watamsikiaje bila mtu kuwahubiria?
15 [a]Nao watahubirije wasipopelekwa?
Kama ilivyoandikwa, "Tazama jinsi ilivyo
mizuri miguu yao wale wanaohubiri habari
njema!"
16 [b]Lakini si wote waliotii Habari Njema.
Kwa maana Isaya asema, "Bwana, ni nani
aliyeamini ujumbe wetu?" 17 [c]Basi, imani
chanzo chake ni kusikia, na kusikia huja
kwa neno la Kristo. 18 [d]Lakini nauliza: Je,
wao hawakusikia? Naam, wamesikia, kwa
maana:

"Sauti yao imeenea duniani pote,
nayo maneno yao yameenea
hadi miisho ya ulimwengu."

19 [e]Nami nauliza tena: Je, Waisraeli
hawakuelewa? Kwanza, Mose asema,

"Nitawafanya mwe na wivu
kwa watu wale ambao si taifa.
Nitawakasirisha kwa taifa
lile lisilo na ufahamu."

20 [f]Naye Isaya kwa ujasiri mwingi anasema,

"Nimeonekana na watu wale ambao
hawakunitafuta.
Nilijifunua kwa watu
wale ambao hawakunitafuta."

21 [g]Lakini kuhusu Israeli anasema,

"Mchana kutwa nimewanyooshea
watu wakaidi na wasiotii mikono
yangu."

### *Mabaki Ya Israeli*

11 [h]Basi nauliza: Je, Mungu amewakataa
watu wake? La, hasha! Mimi
mwenyewe ni Mwisraeli, tena uzao wa
Abrahamu kutoka kabila la Benyamini.
2 [i]Mungu hajawakataa watu wake, ambao
yeye aliwajua tangu mwanzo. Je, hamjui
yale Maandiko yasemayo kuhusu Eliya,
jinsi alivyomlalamikia Mungu kuhusu
Israeli? 3 [j]Alisema, "Bwana, wamewaua
manabii wako na kuzibomoa madhabahu
zako, nimebaki mimi peke yangu, nao
wanataka kuniua?" 4 [k]Je, Mungu alimjibuje?
"Nimejibakizia watu elfu saba ambao
hawajapiga magoti kumwabudu Baali."
5 [l]Vivyo hivyo pia, sasa wapo mabaki
waliochaguliwa kwa neema ya Mungu.
6 [m]Lakini ikiwa wamechaguliwa kwa neema,
si tena kwa msingi wa matendo. Kama
ingekuwa kwa matendo, neema isingekuwa
neema tena.
7 [n]Tuseme nini basi? Kile kitu ambacho
Israeli alikitafuta kwa bidii hakukipata.
Lakini waliochaguliwa walikipata.
Waliobaki walifanywa wagumu, 8 [o]kama
ilivyoandikwa:

"Mungu aliwapa bumbuazi la mioyo,
macho ili wasiweze kuona,
na masikio ili wasiweze kusikia,
hadi leo."

9 [p]Naye Daudi anasema:

"Karamu zao na ziwe tanzi na mtego
wa kuwanasa,
kitu cha kuwakwaza waanguke, na
adhabu kwao.
10 [q]Macho yao yatiwe giza ili wasiweze
kuona,
nayo migongo yao iinamishwe
daima."

### *Matawi Yaliyopandikizwa*

11 [r]Hivyo nauliza tena: Je, Waisraeli
walijikwaa ili waanguke na kuangamia
kabisa? La, hasha! Lakini kwa sababu ya

---

[a]**10:15** Isa 52:7
[b]**10:16** Isa 53:1
[c]**10:17** Gal 3:2, 5; Kol 3:16
[d]**10:18** Za 19:4; Mt 24:14
[e]**10:19** Rum 11:11, 14; Kut 32:21
[f]**10:20** Isa 65:1; Rum 9:20
[g]**10:21** Isa 65:2; Yer 35:17
[h]**11:1** Law 26:46; Za 94:14; 2Kor 11:22; Flp 3:5
[i]**11:2** Rum 8:29; 11:1; 1Fal 19:10, 14
[j]**11:3** 1Fal 19:10, 14
[k]**11:4** 1Fal 19:18
[l]**11:5** Rum 9:27; 3:24
[m]**11:6** Rum 4:4; Gal 3:18
[n]**11:7** Rum 9:31; 9:18
[o]**11:8** Mt 13:13-15; Kum 29:4; Isa 29:10
[p]**11:9** Za 69:22, 23; 35:8
[q]**11:10** Za 69:22, 23; Rum 11:8
[r]**11:11** Mdo 13:46; Rum 10:19; 11:1

makosa yao, wokovu umewafikia watu wa
Mataifa, ili kuwafanya Waisraeli waone
wivu. 12 [a]Basi ikiwa kukosa kwao kumekuwa
utajiri mkubwa kwa ulimwengu, tena kama
kuangamia kwao kumeleta utajiri kwa watu
wa Mataifa, kurudishwa kwao kutaleta
utajiri mkuu zaidi.

13 [b]Sasa ninasema nanyi watu wa Mataifa.
Maadamu mimi ni mtume kwa watu wa
Mataifa, naitukuza huduma yangu 14 [c]ili
kuwafanya watu wangu waone wivu na
hivyo kuwaokoa baadhi yao. 15 [d]Kwa kuwa
ikiwa kukataliwa kwao ni kupatanishwa
kwa ulimwengu, kukubaliwa kwao si
kutakuwa ni uhai baada ya kufa? 16 [e]Kama
sehemu ya donge la unga uliotolewa kuwa
limbuko ni mtakatifu, basi unga wote ni
mtakatifu, nalo shina kama ni takatifu,
vivyo hivyo na matawi nayo.

17 [f]Lakini kama baadhi ya matawi
yalikatwa, nawe chipukizi la mzeituni
mwitu ukapandikizwa mahali pao ili
kushiriki unono pamoja na matawi mengine
kutoka shina la mzeituni, 18 [g]basi usijivune
juu ya hayo matawi. Kama ukijivuna,
kumbuka jambo hili: si wewe unayelishikilia
shina, bali ni shina linalokushikilia wewe.
19 Basi utasema, "Matawi yale yalikatwa
ili nipate kupandikizwa katika hilo shina."
20 [h]Hii ni kweli. Matawi hayo yalikatwa kwa
sababu ya kutokuamini kwake, lakini wewe
umesimama tu kwa sababu ya imani. Kwa
hiyo usijivune, bali simama kwa kuogopa.
21 Kwa maana kama Mungu hakuyahurumia
matawi ya asili, wala hatakuhurumia wewe.

22 [i]Angalia basi wema na ukali wa
Mungu: Kwa wale walioanguka, ukali,
bali kwako wewe wema wa Mungu, kama
utadumu katika wema wake. La sivyo, nawe
utakatiliwa mbali. 23 [j]Wao nao wasipodumu
katika kutokuamini kwao, watapandikizwa
tena kwenye shina, kwa maana Mungu anao
uwezo wa kuwapandikiza tena kwenye hilo
shina. 24 [k]Ikiwa wewe ulikatwa kutoka kile
ambacho kwa asili ni mzeituni mwitu na
kupandikizwa kinyume cha asili kwenye
mzeituni uliopandwa, si rahisi zaidi matawi
haya ya asili kupandikizwa tena kwenye
shina lake la mzeituni!

*Israeli Wote Wataokolewa*

25 [l]Ndugu zangu, ili msije mkajidai kuwa
wenye hekima kuliko mlivyo, nataka
mfahamu siri hii: Ugumu umewapata Israeli
kwa sehemu hadi idadi ya watu wa Mataifa
watakaoingia itimie. 26 [m]Hivyo Israeli wote
wataokolewa. Kama ilivyoandikwa:

"Mkombozi atakuja kutoka Sayuni;
ataondoa kutokumcha Mungu
katika Yakobo.
27 [n]Hili ndilo agano langu nao
nitakapoziondoa dhambi zao."

28 [o]Kwa habari ya Injili, wao ni adui
wa Mungu kwa ajili yenu, lakini kuhusu
kule kuteuliwa kwao ni wapendwa, kwa
ajili ya mababa zao wa zamani, 29 [p]kwa
maana akishawapa watu karama, Mungu
haziondoi, wala wito wake. 30 [q]Kama vile
ninyi wakati fulani mlivyokuwa waasi kwa
Mungu lakini sasa mmepata rehema kwa
sababu ya kutokutii kwao, 31 hivyo nao
Waisraeli wamekuwa waasi ili kwamba
wao nao sasa waweze kupata rehema kwa
ajili ya rehema za Mungu kwenu. 32 [r]Kwa
maana Mungu amewafunga wanadamu
wote kwenye kuasi ili apate kuwarehemu
wote.

[a]**11:12** Rum 11:25
[b]**11:13** Mdo 9:15
[c]**11:14** 1Kor 10:33; 1The 2:16; Mt 1:21; Lk 2:11
[d]**11:15** Rum 5:10; Lk 15:24, 32
[e]**11:16** Law 23:10, 17; Hes 15:18-21
[f]**11:17** Yer 11:16; Yn 15:2; Mdo 2:39; Efe 2:11-13
[g]**11:18** Yn 4:22; 1Kor 10:12
[h]**11:20** 1Kor 10:12; 2Kor 1:24; Rum 12:16; 1Tim 6:17; 1Pet 1:17
[i]**11:22** Rum 2:4; Ebr 3:6; Yn 15:2
[j]**11:23** 2Kor 3:16
[k]**11:24** Yer 11:16
[l]**11:25** Rum 1:13; 1Kor 10:1; 12:1; 2Kor 1:8; 1The 4:13; Rum 12:16; Lk 21:24
[m]**11:26** Isa 45:17; Yer 31:34
[n]**11:27** Isa 59:20, 21; 27; 9; Ebr 8:10, 12
[o]**11:28** Rum 5:10; Kum 7:8; 10:15; Rum 9:5
[p]**11:29** Rum 8:28; Ebr 7:21
[q]**11:30** Efe 2:2; Kol 3:7
[r]**11:32** Rum 3:9; Gal 3:22; 1Tim 2:4

### *Wimbo Wa Shukrani*

33 [a]Tazama jinsi kilivyo kina cha utajiri
wa hekima na maarifa ya Mungu!
Tazama jinsi ambavyo hukumu zake
hazichunguziki,
na ambavyo njia zake
zisivyotafutikana!
34 [b]“Ni nani aliyeyafahamu mawazo ya
Bwana?
Au ni nani ambaye amekuwa
mshauri wake?”
35 [c]“Au ni nani aliyempa chochote
ili arudishiwe?”
36 [d]Kwa maana vitu vyote vyatoka
kwake, viko kwake na kwa
ajili yake.
Utukufu ni wake milele! Amen.

### *Maisha Mapya Katika Kristo*

12 [e]Kwa hiyo, ndugu zangu, nawasihi
kwa rehema zake Mungu, itoeni
miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu
na inayompendeza Mungu, hii ndiyo
ibada yenu yenye maana. 2 [f]Msifuatishe
tena mfano wa ulimwengu huu, bali
mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu.
Ndipo mtaweza kuonja na kuhakikisha
ni nini mapenzi ya Mungu yaliyo mema,
yanayopendeza machoni pake na ukamilifu.
3 [g]Kwa ajili ya neema niliyopewa
nawaambia kila mmoja miongoni mwenu,
asijidhanie kuwa bora kuliko impasavyo,
bali afikiri kwa busara kwa kulingana na
kipimo cha imani Mungu aliyompa. 4 [h]Kama
vile katika mwili mmoja tulivyo na viungo
vingi, navyo viungo vyote havina kazi moja,
5 [i]vivyo hivyo na sisi tulio wengi, tu mwili
mmoja katika Kristo, nasi kila mmoja ni
kiungo cha mwenzake. 6 [j]Tuna karama
zilizotofautiana kila mmoja kutokana na
neema tuliyopewa. Kama ni unabii na
tutoe unabii kwa kadiri ya imani. 7 [k]Kama
ni kuhudumu na tuhudumu, mwenye
kufundisha na afundishe, 8 [l]kama ni kutia
moyo na atie moyo, kama ni kuchangia
kwa ajili ya mahitaji ya wengine na atoe
kwa ukarimu, kama ni uongozi na aongoze
kwa bidii, kama ni kuhurumia wengine na
afanye hivyo kwa furaha.

### *Alama Za Mkristo Wa Kweli*

9 [m]Upendo lazima usiwe na unafiki.
Chukieni lililo ovu, shikamaneni na lililo
jema. 10 [n]Pendaneni ninyi kwa ninyi kwa
upendo wa ndugu. Waheshimuni na
kuwatanguliza wengine. 11 [o]Msiwe wavivu,
bali mwe na bidii katika roho mkimtumikia
Bwana. 12 [p]Kuweni na furaha katika tumaini,
katika dhiki kuweni na saburi, dumuni
katika maombi. 13 [q]Changieni katika
mahitaji ya watakatifu, wakaribisheni
wageni.
14 Wabarikini wale wanaowatesa,
barikini wala msilaani. 15 Furahini pamoja
na wenye kufurahi, lieni pamoja na wale
waliao. 16 Kaeni kwa amani ninyi kwa ninyi.
Msijivune, bali mwe tayari kushirikiana
na wanyonge. Wala msiwe watu wenye
kujivuna kwamba mnajua kila kitu.
17 [r]Msimlipe mtu yeyote ovu kwa ovu.

---

[a]**11:33** Rum 2:4; Mhu 8:17; Efe 3:10; Kol 2:3; Za 92:5; 139:6; Isa 40:28
[b]**11:34** Isa 40:13, 14; Ay 15:8; 36:22; Yer 23:18; 1Kor 2:16
[c]**11:35** Ay 41:11; 35:7
[d]**11:36** 1Kor 8:6; 11:12; Kol 1:16; 1Pet 5:11; 1Tim 1:17; Ebr 2:10; Efe 3:21; Rum 16:27; Yud 25; Ufu 5:13
[e]**12:1** Rum 6:13, 16, 19; 1Kor 6:20; 1Pet 2:5
[f]**12:2** 1Pet 1:14; Efe 5:17; 1Kor 1:20; 2Kor 10; 2; 1Yn 2:15; 1Tim 5:4
[g]**12:3** Rum 15:15; Gal 2:9; 1Kor 15:10; Efe 3:7; 4:7; 1Pet 4:10, 11
[h]**12:4** 1Kor 12:12-14; Efe 4:16
[i]**12:5** 1Kor 6:15; 10:17; 12:12, 20, 27; Efe 2:16; 4:4, 25; Kol 3:15
[j]**12:6** 1Kor 7:7; 12:4, 8-10; Efe 4:11; 1Pet 4:10, 11
[k]**12:7** Efe 4:11; 1Pet 4:10, 11; Mdo 13:1; Efe 4:11
[l]**12:8** Mdo 11:23; 13:15; 15:32; 2Kor 8:2; 9:5-13
[m]**12:9** 2Kor 6:6; 1Tim 1:5; Za 97:10; Amo 5:15; 1The 5:21, 22
[n]**12:10** Za 133:1; 1The 4:9; Ebr 13:1; 1Pet 1:22; Flp 2:3
[o]**12:11** Mdo 18:25; Ufu 3:15
[p]**12:12** Rum 5:2; Ebr 10:32, 36; Lk 18:1
[q]**12:13** Mdo 24:17; 2Fal 4:10; Ay 31:32; 1Tim 3:2; 5:10
[r]**12:17** Mit 20:22; 24:29; 2Kor 8:21

Jitahidini ili mtende yaliyo mema machoni
pa watu wote. 18 [a]Kama ikiwezekana, kwa
upande wenu kaeni kwa amani na watu
wote. 19 [b]Wapendwa, msilipize kisasi,
bali ipisheni ghadhabu ya Mungu, maana
imeandikwa: "Ni juu yangu kulipiza kisasi,
nitalipiza," asema Bwana. 20 [c]Badala yake:

"Kama adui yako ana njaa, mlishe;
kama ana kiu, mpe kinywaji.
Kwa kufanya hivyo,
unaweka makaa ya moto
yanayowaka kichwani pake."

21 Usishindwe na ubaya, bali uushinde
ubaya kwa wema.

*Kutii Mamlaka*

13 [d]Kila mtu na atii mamlaka inayotawala,
kwa maana hakuna mamlaka isiyotoka
kwa Mungu, nazo mamlaka zilizopo
zimewekwa na Mungu. 2 [e]Kwa hiyo yeye
anayeasi dhidi ya mamlaka inayotawala
anaasi dhidi ya kile kilichowekwa na Mungu,
nao wale wafanyao hivyo watajiletea
hukumu juu yao wenyewe. 3 [f]Kwa kuwa
watawala hawawatishi watu wale
wanaotenda mema bali wale wanaotenda
mabaya. Je, wataka usimwogope mwenye
mamlaka? Basi tenda lile lililo jema naye
atakusifu. 4 [g]Kwa maana mwenye mamlaka
ni mtumishi wa Mungu kwa ajili ya mema.
Lakini kama ukitenda mabaya, basi ogopa,
kwa kuwa hauinui upanga bila sababu.
Yeye ni mtumishi wa Mungu, mjumbe
wa Mungu wa kutekeleza adhabu juu ya
watenda mabaya. 5 [h]Kwa hiyo ni lazima
kutii wenye mamlaka, si kwa sababu ya
kuogopa adhabu iwezayo kutolewa, bali
pia kwa ajili ya dhamiri.

6 [i]Kwa sababu hii mnalipa kodi, kwa
maana watawala ni watumishi wa Mungu,
ambao hutumia muda wao wote kutawala.
7 [j]Mlipeni kila mtu kile mnachodaiwa.
Kama mnadaiwa kodi lipeni kodi, kama
ni ushuru, lipeni ushuru, astahiliye hofu,
mhofu, astahiliye heshima, mheshimu.

*Kupendana Kila Mmoja Na Mwingine*

8 [k]Msidaiwe kitu na mtu yeyote, isipokuwa
kupendana, kwa maana yeye ampendaye
mwenzake, ameitimiza sheria. 9 [l]Kwa kuwa
amri hizi zisemazo, "Usizini," "Usiue,"
"Usiibe," "Usitamani," na amri nyingine
zote, zinajumlishwa katika amri hii moja:
"Mpende jirani yako kama nafsi yako."
10 [m]Upendo haumfanyii jirani jambo baya.
Kwa hiyo upendo ndio utimilifu wa sheria.
11 [n]Nanyi fanyeni hivi, mkiutambua
wakati tulio nao. Saa ya kuamka kutoka
usingizini imewadia, kwa maana sasa
wokovu wetu umekaribia zaidi kuliko hapo
kwanza tulipoamini. 12 [o]Usiku umeendelea
sana, mapambazuko yamekaribia. Kwa hiyo
tuyaweke kando matendo ya giza na tuvae
silaha za nuru. 13 [p]Basi na tuenende kwa
adabu kama inavyopasa wakati wa mchana,
si kwa kufanya karamu za ulafi na ulevi, si
kwa ufisadi na uasherati, si kwa ugomvi na
wivu. 14 [q]Bali jivikeni Bwana Yesu Kristo,
wala msifikiri jinsi mtakavyotimiza tamaa
za miili yenu yenye asili ya dhambi.

*Msiwahukumu Wengine*

14 [r]Mkaribisheni yeye ambaye imani yake
ni dhaifu, lakini si kwa kugombana

---

[a]**12:18** Mk 9:50; Rum 14:19
[b]**12:19** Law 19:18; Mit 20:22; 22:29; Kum 32:35; Mwa 50:19; Isa 26:10
[c]**12:20** Kut 23:4; Mt 5:44; Mit 25:21, 22; Lk 6:27
[d]**13:1** Tit 3:1; 1Pet 2:13, 14; Dan 2:21; 4:17; Yn 19:11
[e]**13:2** Kut 16:8; Tit 3:1
[f]**13:3** 1Pet 2:14; 3:13
[g]**13:4** 1The 4:6; Za 82:6; Rum 12:19
[h]**13:5** Mit 24:21, 22; Mhu 8:2; 1Pet 2:19
[i]**13:6** Mt 22:17
[j]**13:7** Mt 17:25; 22:17, 21; Lk 23:2
[k]**13:8** Mt 5:43; Yn 13:34; Kol 3:14
[l]**13:9** Kut 20:13-15; Kum 5:17; 19:21; Law 19:18; Mt 17:19
[m]**13:10** Mt 22:39, 40; 1Kor 13:4; Rum 13:8, 9
[n]**13:11** Yak 5:8; 1Pet 4:7; Efe 5:14; 1The 5:5, 6
[o]**13:12** Ebr 10:25; 1Yn 2:8; Efe 5:11; 6:11, 13; 1The 5:8
[p]**13:13** Efe 5:18; Lk 21:34; Gal 5:20, 21; 1Pet 4:3
[q]**13:14** Gal 5:16
[r]**14:1** 1Kor 8:9-12; 9:22

na kubishana juu ya mawazo yake. 2 [a]Mtu
mmoja imani yake inamruhusu kula kila
kitu, lakini mwingine ambaye imani yake
ni dhaifu, hula mboga tu. 3 [b]Yeye alaye kila
kitu asimdharau yeye asiyekula. Wala yeye
asiyekula kila kitu asimhukumu yule alaye
kila kitu, kwa maana Mungu amemkubali.
4 [c]Wewe ni nani hata umhukumu mtumishi
wa mtu mwingine? Kwa bwana wake tu
anasimama au kuanguka. Naye atasimama
kwa sababu Bwana anaweza kumsimamisha.

5 [d]Mtu mmoja anaitukuza siku fulani
kuwa ni bora kuliko nyingine, na mwingine
anaona kuwa siku zote ni sawa. Basi kila
mmoja awe na hakika na yale anayoamini.
6 [e]Yeye anayehesabu siku moja kuwa
takatifu kuliko nyingine, hufanya hivyo kwa
kumheshimu Bwana. Naye alaye nyama
hula kwa Bwana, kwa maana humshukuru
Mungu, naye akataaye kula nyama hufanya
hivyo kwa Bwana na humshukuru Mungu.
7 [f]Kwa kuwa hakuna hata mmoja wetu
anayeishi kwa ajili yake mwenyewe, wala
hakuna hata mmoja wetu afaye kwa ajili
yake mwenyewe. 8 [g]Kama tunaishi, tunaishi
kwa Bwana, nasi pia tukifa tunakufa kwa
Bwana. Kwa hiyo basi, kama tukiishi au
kama tukifa, sisi ni mali ya Bwana.

9 [h]Kwani kwa sababu hii hasa, Kristo
alikufa na akawa hai tena kusudi apate
kuwa Bwana wa wote, yaani, waliokufa
na walio hai. 10 [i]Basi kwa nini wewe
wamhukumu ndugu yako? Au kwa nini
wewe unamdharau ndugu yako? Kwa kuwa
sote tutasimama mbele ya kiti cha Mungu
cha hukumu. 11 [j]Kwa kuwa imeandikwa:

"'Kama vile niishivyo,' asema
Bwana,
'kila goti litapigwa mbele zangu,
na kila ulimi utakiri kwa Mungu.'"

12 [k]Hivyo basi kila mmoja wetu atatoa
habari zake mwenyewe kwa Mungu.

*Usimfanye Ndugu Yako Ajikwae*

13 [l]Kwa hiyo tusiendelee kuhukumiana:
Badala yake mtu asiweke kamwe kikwazo
au kizuizi katika njia ya ndugu mwingine.
14 [m]Ninajua tena nimehakikishiwa sana
katika Bwana Yesu kwamba hakuna kitu
chochote ambacho ni najisi kwa asili yake.
Lakini kama mtu anakiona kitu kuwa ni
najisi, basi kwake huyo kitu hicho ni najisi.
15 [n]Kama ndugu yako anahuzunishwa kwa
sababu ya kile unachokula, basi huenendi
tena katika upendo. Usiruhusu kile
unachokula kiwe sababu ya kumwangamiza
ndugu yako ambaye Kristo alikufa kwa ajili
yake. 16 [o]Usiruhusu kile ambacho unakiona
kuwa chema kisemwe kuwa ni kiovu.
17 [p]Kwa maana Ufalme wa Mungu si kula
na kunywa, bali ni haki, amani na furaha
katika Roho Mtakatifu. 18 [q]Kwa sababu mtu
yeyote anayemtumikia Kristo kwa jinsi hii,
anampendeza Mungu na kukubaliwa na
wanadamu.

19 [r]Kwa hiyo na tufanye bidii kutafuta
yale yaletayo amani na kujengana sisi
kwa sisi. 20 [s]Usiiharibu kazi ya Mungu
kwa ajili ya chakula. Hakika vyakula vyote
ni safi, lakini ni kosa kula kitu chochote
kinachomsababisha ndugu yako ajikwae.
21 [t]Ni afadhali kutokula nyama wala
kunywa divai au kufanya jambo lingine

[a]**14:2** Rum 14:14; 1Kor 10:25; 1Tim 4:4; Tit 1:15
[b]**14:3** Lk 18:9; Kol 2:16
[c]**14:4** Mt 7:1; Yak 4:12
[d]**14:5** Gal 4:10; Kol 2:16
[e]**14:6** Mt 14:19; 1Tim 4:3, 4
[f]**14:7** 2Kor 5:15; Gal 2:20
[g]**14:8** Flp 1:20; Gal 2:20; 1The 5:10; Lk 20:38
[h]**14:9** Ufu 1:18; 2:8; Mdo 10:42; 2Kor 5:15
[i]**14:10** 2Kor 5:10; Mdo 17:31; Mt 25:31, 32; 7:1; 2Kor 5:10
[j]**14:11** Isa 45:23; Flp 2:10, 11
[k]**14:12** Mt 12:36; 1Pet 4:5
[l]**14:13** Mt 7:1; Rum 14:1; 2Kor 8:9, 13
[m]**14:14** Mdo 10:15; 1Kor 8:7
[n]**14:15** Efe 5:2; 1Kor 8:7
[o]**14:16** 1Kor 10:30; Tit 2:5; Rum 12:17
[p]**14:17** 1Kor 8:8; Gal 5:22
[q]**14:18** Lk 2:52; Mdo 24:16
[r]**14:19** Za 34:14; 1Kor 7:15; Rum 15:2; Efe 4:12, 29
[s]**14:20** Rum 14:15; Mt 15:11; Mdo 10:15; Tit 1:15
[t]**14:21** 1Kor 8:13; Mt 15:29

lolote litakalomsababisha ndugu yako
ajikwae.
22 [a]Je, wewe unayo imani? Ile imani
uliyo nayo, uwe nayo nafsini mwako
mbele za Mungu. Heri mtu yule asiye na
sababu ya kujihukumu nafsi yake kwa
ajili ya kile anachokifanya. 23 Lakini kama
mtu ana shaka kuhusu kile anachokula,
amehukumiwa, kwa sababu hakula kwa
imani. Kwa kuwa chochote kinachofanywa
pasipo imani ni dhambi.

### *Usijipendeze Mwenyewe, Bali Wapendeze Wengine*

15 [b]Sisi tulio na nguvu, hatuna budi
kuchukuliana na kushindwa kwa wale
walio dhaifu wala si kujipendeza nafsi zetu
wenyewe. 2 [c]Kila mmoja wetu inampasa
kumpendeza jirani yake kwa mambo mema,
ili kumjenga katika imani. 3 [d]Kwa maana
hata Kristo hakujipendeza mwenyewe, bali
kama ilivyoandikwa: “Matukano yao wale
wanaokutukana wewe yalinipata mimi.”
4 [e]Kwa maana kila kitu kilichoandikwa
zamani, kiliandikwa kutufundisha, ili
kwamba kwa saburi na faraja tunayopata
katika Maandiko tuwe na tumaini.
5 [f]Mungu atoaye saburi na faraja, awajalie
ninyi roho ya umoja miongoni mwenu
mnapomfuata Kristo Yesu, 6 [g]ili kwa moyo
mmoja mpate kumtukuza Mungu aliye Baba
wa Bwana wetu Yesu Kristo.

### *Injili Sawa Kwa Wayahudi Na Kwa Watu Wa Mataifa*

7 [h]Karibishaneni ninyi kwa ninyi kama
Kristo alivyowakaribisha ninyi ili kumletea
Mungu utukufu. 8 [i]Kwa maana nawaambia
kwamba, Kristo amekuwa mtumishi kwa
wale waliotahiriwa ili kuonyesha kweli
ya Mungu na kuthibitisha zile ahadi
walizopewa baba zetu wa zamani, 9 [j]pia
ili watu wa Mataifa wamtukuze Mungu kwa
rehema zake. Kama ilivyoandikwa:

> “Kwa hiyo nitakutukuza katikati ya
> watu wa Mataifa;
> nitaliimbia sifa jina lako.”

10 [k]Tena yasema,

> “Enyi watu wa Mataifa, furahini
> pamoja na watu wa Mungu.”

11 [l]Tena,

> “Msifuni Bwana, ninyi watu wa
> Mataifa wote,
> na kumwimbia sifa, enyi watu
> wote.”

12 [m]Tena Isaya anasema,

> “Shina la Yese litachipuka,
> yeye atakayeinuka ili kutawala juu
> ya mataifa.
> Watu wa Mataifa watamtumaini.”

13 [n]Mungu wa tumaini awajaze ninyi
furaha yote na amani katika kumwamini,
ili mpate kujawa na tumaini tele kwa nguvu
ya Roho Mtakatifu.

### *Paulo Mhudumu Wa Watu Wa Mataifa*

14 [o]Ndugu zangu, mimi mwenyewe
ninasadiki kwamba mmejaa wema na
ufahamu wote, tena mnaweza kufundishana
ninyi kwa ninyi. 15 [p]Nimewaandikia kwa
ujasiri vipengele kadha wa kadha katika
waraka huu kama kuwakumbusha tena
kwa habari ya ile neema Mungu aliyonipa,
16 [q]ili kuwa mhudumu wa Kristo Yesu kwa
watu wa Mataifa nikiwa na huduma ya
kikuhani ya kutangaza Injili ya Mungu, ili
watu wa Mataifa wapate kuwa dhabihu

---

[a]**14:22** 1Yn 3:21; Mt 15:29
[b]**15:1** Rum 14:1; 1The 5:14
[c]**15:2** 1Kor 10:33
[d]**15:3** 2Kor 8:9; Za 69:9
[e]**15:4** Rum 4:23, 24; 1Kor 10:11; 9:9, 10; 10:11; 2Tim 3:16, 17
[f]**15:5** 2Kor 13:11; Efe 4:3
[g]**15:6** Ufu 1; 6; Za 34:3; Mdo 4:24, 32
[h]**15:7** Rum 14:1; 5:2
[i]**15:8** Mt 15:24; Mdo 3:25, 26; 2Kor 1:20
[j]**15:9** Rum 3:29; Mt 9:8; 2Sam 22:50; Za 18:49
[k]**15:10** Kum 32:43
[l]**15:11** Za 117:1
[m]**15:12** Ufu 5:5; Isa 11:10; Mt 12:21
[n]**15:13** Rum 14:17; 1Kor 4:20
[o]**15:14** Efe 5:9; 2Pet 1:12
[p]**15:15** Rum 12:3; 1:5; 12:3; Gal 1:15; Efe 3:7, 8
[q]**15:16** Mdo 9:5; Rum 11:13; 1:1; Isa 66:20

inayokubaliwa na Mungu, iliyotakaswa na
Roho Mtakatifu.
17 [a]Kwa hiyo ninajisifu katika Kristo Yesu,
kwenye utumishi wangu kwa Mungu. 18 [b]Kwa
maana sitathubutu kusema kitu chochote
zaidi ya kile ambacho Kristo amefanya
kwa kunitumia mimi katika kuwaongoza
watu wa Mataifa wamtii Mungu kwa yale
niliyosema na kufanya, 19 [c]kwa nguvu za
ishara na miujiza, kwa uweza wa Roho
wa Mungu, hivyo kuanzia Yerusalemu
hadi maeneo yote ya kandokando yake
mpaka Iliriko, nimekwisha kuihubiri Injili
ya Kristo kwa ukamilifu. 20 [d]Hivyo ni nia
yangu kuhubiri Habari Njema, si pale
ambapo Kristo amekwisha kujulikana,
ili nisije nikajenga juu ya msingi wa mtu
mwingine. 21 [e]Lakini kama ilivyoandikwa:

> “Wale ambao hawajahubiriwa habari
> zake wataona,
> nao wale ambao hawajazisikia
> watafahamu.”

22 [f]Hii ndiyo sababu nimezuiliwa mara
nyingi nisiweze kuja kwenu.

*Paulo Apanga Kwenda Rumi*

23 [g]Lakini sasa kwa kuwa hakuna nafasi
zaidi kwa ajili yangu katika sehemu hii,
ninatamani kuja kwenu kama ambavyo
nimekuwa na shauku kwa miaka mingi.
24 [h]Nimekusudia kufanya hivyo nitakapokuwa
njiani kwenda Hispania. Natarajia kuwaona
katika safari yangu na kusafirishwa nanyi
mpaka huko, baada ya kufurahia ushirika
wenu kwa kitambo kidogo. 25 [i]Sasa, niko
njiani kuelekea Yerusalemu kwa ajili ya
kuwahudumia watakatifu huko. 26 [j]Kwa
kuwa imewapendeza watu wa Makedonia
na Akaya kufanya changizo kwa ajili ya
maskini walioko miongoni mwa watakatifu
huko Yerusalemu. 27 [k]Imewapendeza
kufanya hivyo, naam, kwani ni wadeni
wao. Kwa maana ikiwa watu wa Mataifa
wameshiriki baraka za rohoni za Wayahudi,
wao ni wadeni wa Wayahudi, ili Wayahudi
nao washiriki baraka zao za mambo ya
mwilini. 28 [l]Kwa hiyo baada ya kukamilisha
kazi hii na kuhakikisha kuwa wamepokea
kila kitu kilichokusanywa, nitapitia kwenu
nikiwa njiani kwenda Hispania. 29 [m]Ninajua
kwamba nitakapokuja kwenu, nitakuja na
wingi wa baraka za Kristo.
30 [n]Basi, ndugu zangu, nawasihi kwa Jina
la Bwana wetu Yesu Kristo na kwa upendo
wa Roho Mtakatifu, kujiunga nami katika
taabu zangu mkiniombea kwa Mungu.
31 [o]Ombeni ili nipate kuokolewa mikononi
mwa wale wasioamini walioko Uyahudi, na
kwamba utumishi wangu upate kukubaliwa
na watakatifu wa huko Yerusalemu, 32 [p]ili
kwa mapenzi ya Mungu niweze kuja kwenu
kwa furaha, nami niburudishwe pamoja
nanyi. 33 [q]Mungu wa amani na awe pamoja
nanyi nyote. Amen.

*Salamu Kwa Watu Binafsi*

16 [r]Napenda kumtambulisha kwenu dada
yetu Foibe, mtumishi katika kanisa la
Kenkrea. 2 [s]Naomba mpokeeni katika Bwana
ipasavyo watakatifu na kumpa msaada
wowote atakaohitaji kutoka kwenu, kwa
maana yeye amekuwa msaada kwa watu
wengi, mimi nikiwa miongoni mwao.

> 3 [t]Wasalimuni Prisila[u] na Akila,
> watumishi wenzangu katika
> Kristo Yesu. 4 Wao walihatarisha
> maisha yao kwa ajili yangu; wala

---

[a]**15:17** Flp 3:3; Ebr 2:17
[b]**15:18** Mdo 15:12; Rum 1:15; 16:26
[c]**15:19** Yn 4:48; Mdo 19:11; 22:17-21
[d]**15:20** 2Kor 10:15, 16
[e]**15:21** Isa 52:15
[f]**15:22** Rum 1:13
[g]**15:23** Mdo 19:21; 24:17
[h]**15:24** Rum 15:28; 1Kor 16:6; Tit 3:1
[i]**15:25** Mdo 19:21; 24:17
[j]**15:26** Rum 16:9; 2Kor 1:11; Kol 4:12
[k]**15:27** 1Kor 9:11; Rum 9:4; 11:17; Gal 6:6
[l]**15:28** Flp 4:17; Rum 15:24
[m]**15:29** Rum 1:10; 1:11
[n]**15:30** Gal 5:22; 2Kor 1:11; Kol 4:12
[o]**15:31** 2Kor 1:10; 2Tim 3:11
[p]**15:32** Mdo 18:21; Rum 1:10, 13; 1Kor 16:18
[q]**15:33** 2The 3:16
[r]**16:1** 2Kor 3:1; Mdo 18:18
[s]**16:2** Flp 2:29; 3Yn 5, 6; Mdo 9:13
[t]**16:3** Mdo 18:2; Gal 5:6; Rum 8:1
[u]3 Prisila kwa Kiyunani ni Priska, hivyo tafsiri nyingine zimemuita Priska.

si mimi tu ninayewashukuru bali pia makanisa yote ya watu wa Mataifa.
5 [a]Lisalimuni pia kanisa linalokutana nyumbani mwao.
Msalimuni rafiki yangu mpendwa Epaineto, aliyekuwa mtu wa kwanza kumwamini Kristo huko Asia.
6 Msalimuni Maria, aliyefanya kazi kwa bidii kwa ajili yenu.
7 [b]Wasalimuni Androniko na Yunia, jamaa zangu ambao wamekuwa gerezani pamoja nami. Wao ni maarufu miongoni mwa mitume, nao walikuwa katika Kristo kabla yangu.
8 Msalimuni Ampliato, yeye nimpendaye katika Bwana.
9 [c]Msalimuni Urbano, mtendakazi mwenzetu katika Kristo, pamoja na rafiki yangu mpendwa Stakisi.
10 [d]Msalimuni Apele aliyejaribiwa na akaithibitisha imani yake katika Kristo.
Wasalimuni wote walio nyumbani mwa Aristobulo.
11 [e]Msalimuni ndugu yangu Herodioni.
Wasalimuni wote walio nyumbani mwa Narkisi walio katika Bwana.
12 Wasalimuni Trifaina na Trifosa, wale wanawake wanaofanya kazi kwa bidii katika Bwana.
Msalimuni rafiki yangu mpendwa Persisi, mwanamke mwingine aliyefanya kazi kwa bidii katika Bwana.
13 [f]Msalimuni Rufo, mteule katika Bwana, pamoja na mama yake, ambaye amekuwa mama kwangu pia.
14 Wasalimuni Asinkrito, Flegoni, Herme, Patroba, Herma na ndugu wote walio pamoja nao.
15 [g]Wasalimuni Filologo, Yulia, Nerea na dada yake, na Olimpa na watakatifu wote walio pamoja nao.
16 [h]Salimianeni ninyi kwa ninyi kwa busu takatifu.
Makanisa yote ya Kristo yanawasalimu.

*Maelekezo Ya Mwisho*

17 [i]Ndugu zangu, nawasihi mjihadhari
na kujiepusha na wale watu waletao
matengano na kuweka vikwazo mbele yenu
dhidi ya mafundisho mliyojifunza. 18 [j]Kwa
maana watu kama hao hawamtumikii
Bwana Kristo, bali wanatumikia tamaa zao
wenyewe. Kwa kutumia maneno laini na ya
kubembeleza, hupotosha mioyo ya watu
wajinga. 19 [k]Kila mtu amesikia juu ya utii
wenu, nami nimejawa na furaha tele kwa
ajili yenu. Lakini nataka mwe na hekima
katika mambo mema na bila hatia katika
mambo maovu.
20 [l]Mungu wa amani atamponda Shetani
chini ya miguu yenu upesi.
Neema ya Bwana wetu Yesu iwe nanyi.
Amen.
21 [m]Timotheo, mtendakazi mwenzangu
anawasalimu. Vivyo hivyo Lukio, Yasoni,
na Sosipatro, ndugu zangu.
22 Mimi, Tertio, niliye mwandishi wa
waraka huu, nawasalimu katika Bwana.
23 [n]Gayo, ambaye ni mwenyeji wangu na
wa kanisa lote, anawasalimu.
Erasto, mweka hazina wa mji huu, pamoja
na Kwarto ndugu yetu pia wanawasalimu.
[ 24 [o]Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo
iwe pamoja nanyi nyote. Amen.]

[a]**16:5** Kol 4:15; 1Kor 16:15
[b]**16:7** Gal 1:22
[c]**16:9** Rum 16:3
[d]**16:10** Mdo 11:14
[e]**16:11** Rum 16:7, 21; Mdo 11:14
[f]**16:13** Mk 15:21
[g]**16:15** Mdo 9:13; 16; 2
[h]**16:16** 1The 5:26; 1Pet 5:14
[i]**16:17** 1Tim 1:3; 6:3; Mt 18:15-17; 1Kor 14:20
[j]**16:18** Flp 3:19; Kol 2:4
[k]**16:19** Rum 1:8; Mt 10:16; 1Kor 14:20
[l]**16:20** Rum 15:33; Mwa 3:15
[m]**16:21** Mdo 16:1; 13:1; 17:6
[n]**16:23** Mdo 19:22
[o]**16:24** Rum 16:20; 1The 5:28

*Maneno Ya Mwisho Ya Kumsifu Mungu*

25 [a]Sasa atukuzwe yeye awezaye
kuwafanya ninyi imara kwa Injili yangu na
kuhubiriwa kwa Yesu Kristo, kutokana na
kufunuliwa siri zilizofichika tangu zamani
za kale. 26 [b]Lakini sasa siri hiyo imefunuliwa
na kujulikana kupitia maandiko ya kinabii
kutokana na amri ya Mungu wa milele, ili
mataifa yote yaweze kumwamini na kumtii
27 [c]Mungu aliye pekee, mwenye hekima,
ambaye kwa njia ya Yesu Kristo utukufu
ni wake milele na milele! Amen.

---

[a]**16:25** Flp 3:20; Rum 2:16; Isa 48:6; 1Tim 3:16
[b]**16:26** Efe 1:9; 2Tim 1:10; Tit 1:2, 3; 1Pet 1:20; Mdo 6:7
[c]**16:27** Rum 11:36; 1Tim 1:17; 6:16; Yud 25

# 1 WAKORINTHO

*Salamu*

1 [a]Paulo, niliyeitwa kwa mapenzi ya
Mungu kuwa mtume wa Kristo Yesu, na
Sosthene ndugu yetu.
2 [b]Kwa kanisa la Mungu lililoko Korintho,
kwa wale waliotakaswa katika Kristo Yesu
na walioitwa kuwa watakatifu, pamoja na
wale wote ambao kila mahali wanaliitia
Jina la Kristo Yesu Bwana wetu, aliye
Bwana wao na wetu pia:
3 [c]Neema na amani itokayo kwa Mungu
Baba yetu na kwa Bwana Yesu Kristo iwe
nanyi.

*Shukrani*

4 [d]Ninamshukuru Mungu siku zote kwa
ajili yenu kwa sababu ya neema yake
mliyopewa katika Kristo Yesu. 5 [e]Kwa kuwa
katika Kristo mmetajirishwa kwa kila hali,
katika kusema kwenu na katika maarifa
yenu yote, 6 [f]kwa sababu ushuhuda wetu
kumhusu Kristo ulithibitishwa ndani yenu.
7 [g]Kwa hiyo hamkupungukiwa na karama
yoyote ya kiroho wakati mnangoja kwa
shauku kudhihirishwa kwa Bwana wetu
Yesu Kristo. 8 [h]Atawafanya imara mpaka
mwisho, ili msiwe na hatia siku ile ya
Bwana wetu Yesu Kristo. 9 [i]Mungu ambaye
mmeitwa naye ili mwe na ushirika na
Mwanawe Yesu Kristo, Bwana wetu ni
mwaminifu.

*Mgawanyiko Ndani Ya Kanisa*

10 [j]Nawasihi ndugu zangu, katika Jina la
Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba mpatane
nia zenu ninyi kwa ninyi, ili pasiwepo na
matengano katikati yenu na kwamba mwe
na umoja kikamilifu katika nia na katika
kusudi. 11 [k]Ndugu zangu, nimepata habari
kutoka kwa baadhi ya watu wa nyumbani
mwa Kloe kwamba kuna magomvi katikati
yenu. 12 [l]Maana yangu ni kwamba: Mmoja
wenu husema, “Mimi ni wa Paulo”;
mwingine, “Mimi ni wa Apolo”; mwingine,
“Mimi ni wa Kefa,”[m] na mwingine, “Mimi
ni wa Kristo.”
13 Je, Kristo amegawanyika? Je, Paulo
ndiye alisulubishwa kwa ajili yenu? Je,
mlibatizwa kwa jina la Paulo? 14 [n]Nashukuru
kwamba sikumbatiza mtu yeyote isipokuwa
Krispo na Gayo. 15 Kwa hiyo hakuna
mtu yeyote anayeweza kusema kwamba
alibatizwa kwa jina langu. 16 [o](Naam,
niliwabatiza pia watu wa nyumbani mwa
Stefana. Lakini zaidi ya hao sijui kama
nilimbatiza mtu mwingine yeyote.) 17 [p]Kwa
maana Kristo hakunituma ili kubatiza bali
kuhubiri Injili; sio kwa maneno ya hekima
ya kibinadamu, ili msalaba wa Kristo usije
ukakosa nguvu yake.

*Kristo Ni Hekima Na Nguvu Ya Mungu*

18 [q]Kwa maana ujumbe wa msalaba kwa
wale wanaopotea ni upuzi, lakini kwetu sisi
tunaookolewa ni nguvu ya Mungu. 19 [r]Kwa
maana imeandikwa:

---

[a]**1:1** Rum 1:1; Efe 1:1; 2Kor 1:1; 2Tim 1:1; Mdo 18:17
[b]**1:2** 1Kor 10:32; Mdo 2:21; 18:1; Rum 1:17
[c]**1:3** Rum 1:7; 1Kor 1:2; Efe 1:2; 1Pet 1:2
[d]**1:4** Rum 1:8
[e]**1:5** 2Kor 8:7; 1Kor 12:8; 2Kor 9:11
[f]**1:6** 2The 1:10; 1Tim 2:6; Ufu 1:2
[g]**1:7** Rum 1:11; 1Kor 12:1-3; Mt 16:27; Lk 17:30; Ufu 1:7; 1The 1:10; 2:19; Tit 2:13; Yak 5:7-8; 1Pet 1:13; 2Pet 3:12
[h]**1:8** 1The 3:13; 5:2; Amo 5:18; 1Kor 5:5; Flp 1:6; 2:16
[i]**1:9** Rum 8:28; 1Yn 1:3; Isa 49:7; Kum 7:9; 1Kor 10:13; 1The 3:3; 1Tim 2:13; Ebr 10:23; 11:11
[j]**1:10** Rum 7:1; 15:5; 1Kor 11:18
[k]**1:11** Mdo 11:14
[l]**1:12** 1Kor 3:4-22; Mdo 18:24; Yn 1:42; 1Kor 3:22; 9:5
[m]12 Yaani Petro.
[n]**1:14** Mdo 18:8; 19:29; Rum 16:23
[o]**1:16** Mdo 11:14; 1Kor 16:15
[p]**1:17** Yn 4:2; Mdo 2:38; 1Kor 2:1-13
[q]**1:18** 1Kor 2:14; 2Kor 2:15; 4:3; 2The 2:10; Mdo 2:47; Rum 1:16
[r]**1:19** Isa 29:14; Ay 5:12, 13; Yer 8:9

"Nitaiharibu hekima ya wenye
hekima,
na kubatilisha akili ya wenye
akili."

[20] [a]Yuko wapi mwenye hekima? Yuko
wapi msomi? Yuko wapi mwanafalsafa wa
nyakati hizi? Je, Mungu hakufanya hekima
ya ulimwengu huu kuwa upumbavu?
[21] [b]Kwa kuwa katika hekima ya Mungu,
ulimwengu kwa hekima yake haukumjua
yeye, ilimpendeza Mungu kuwaokoa
wale walioamini kwa upuzi wa lile neno
lililohubiriwa. [22] [c]Wayahudi wanadai
ishara za miujiza na Wayunani wanatafuta
hekima. [23] [d]Lakini sisi tunamhubiri Kristo
aliyesulubiwa: yeye kwa Wayahudi ni
kikwazo na kwa Wayunani ni upuzi.
[24] [e]Lakini kwa wale ambao Mungu amewaita,
Wayahudi na pia Wayunani, Kristo ndiye
nguvu ya Mungu na pia hekima ya Mungu.
[25] [f]Kwa maana upumbavu wa Mungu una
hekima zaidi kuliko hekima ya wanadamu,
nao udhaifu wa Mungu una nguvu kuliko
nguvu ya wanadamu.

[26] [g]Ndugu zangu, kumbukeni mlivyokuwa
mlipoitwa. Kwa kipimo cha kibinadamu, si
wengi wenu mliokuwa na hekima. Si wengi
mliokuwa na ushawishi, si wengi mliozaliwa
katika jamaa zenye vyeo. [27] [h]Lakini Mungu
alivichagua vitu vipumbavu vya ulimwengu
ili awaaibishe wenye hekima, Mungu
alivichagua vitu dhaifu vya ulimwengu ili
awaaibishe wenye nguvu. [28] [i]Alivichagua
vitu vya chini na vinavyodharauliwa
vya dunia hii, vitu ambavyo haviko,
ili avibatilishe vile vilivyoko, [29] [j]ili mtu
yeyote asijisifu mbele zake. [30] [k]Bali kwa
yeye ninyi mmepata kuwa katika Kristo
Yesu, aliyefanyika kwetu hekima itokayo
kwa Mungu, yaani haki, na utakatifu na
ukombozi. [31] [l]Hivyo, kama ilivyoandikwa:
"Yeye ajisifuye na ajisifu katika Bwana."

### *Kumtangaza Kristo Aliyesulubiwa*

**2** [m]Ndugu zangu nilipokuja kwenu, sikuja
na maneno ya ushawishi wala hekima ya
hali ya juu nilipowahubiria siri ya Mungu.
[2] [n]Kwa kuwa niliamua kutokujua kitu
chochote wakati nikiwa nanyi isipokuwa
Yesu Kristo aliyesulubiwa. [3] [o]Mimi nilikuja
kwenu nikiwa dhaifu na mwenye hofu
na kwa kutetemeka sana. [4] [p]Kuhubiri
kwangu na ujumbe wangu haukuwa kwa
hekima na maneno ya ushawishi bali kwa
madhihirisho ya nguvu za Roho [5] ili imani
yenu isiwe imejengwa katika hekima ya
wanadamu bali katika nguvu za Mungu.

### *Hekima Ya Kweli Itokayo Kwa Mungu*

[6] [q]Lakini miongoni mwa watu
waliokomaa twanena hekima, wala si
hekima ya ulimwengu huu au ya watawala
wa dunia hii wanaobatilika. [7] [r]Sisi tunanena
hekima ya Mungu ambayo ni siri, tena
iliyofichika, ambayo Mungu aliikusudia
kabla ya ulimwengu kuwepo, kwa ajili
ya utukufu wetu. [8] [s]Hakuna hata mtawala
mmoja wa nyakati hizi aliyeelewa jambo
hili. Kwa maana kama wangelielewa,
wasingemsulubisha Bwana wa utukufu.
[9] [t]Lakini ni kama ilivyoandikwa:

---

[a]**1:20** Isa 19:11-12; 1Kor 2:6-8; 3:18; 2Kor 4:4; Gal 1:4; Ay 12:17; Isa 44:25; Yer 8:9; Rum 1:22; 1Kor 3:18-19
[b]**1:21** 1Kor 6:2; 11:32; Rum 11:14; 3:22
[c]**1:22** Mt 12:38; Yn 2:11; 4:48
[d]**1:23** 1Kor 2:2; Gal 3:1; Lk 2:34
[e]**1:24** Rum 8:28; 1:16; Kol 2:3
[f]**1:25** 2Kor 13:4; 1Kor 1:18
[g]**1:26** Rum 8:28; 1Kor 1:20; Yn 7:48
[h]**1:27** Yak 2:5; Rum 1:22; 1Kor 3:18-19
[i]**1:28** Rum 4:17; 1Kor 2:6
[j]**1:29** Efe 2:9
[k]**1:30** Rum 16:3; Yer 5:5-6; 33:16; 2Kor 5:21; Flp 3:9; 1Kor 1:2; Rum 3:24
[l]**1:31** Yer 9:23; Za 34:2; 44:8; 2Kor 10:17
[m]**2:1** 1Kor 1:17; 2:4; 13; 2Kor 10:10; 11; 1Kor 1:6
[n]**2:2** Gal 6:14; 1Kor 1:23
[o]**2:3** Mdo 18:1-18; 1Kor 4:10; 9:22; 2Kor 11:29-30; 12:5-10; 13:9; 7:15
[p]**2:4** Rum 15:13; 1Kor 2:1; 1:17; 2Pet 1:16
[q]**2:6** Efe 4:13; Flp 3:15; Kol 4:12; Ebr 5:14; 6:1; Yak 1:4; 1Kor 1:20; Za 146:4
[r]**2:7** Rum 16:25; Efe 3:5, 9; Kol 1:26; 2Tim 1:9
[s]**2:8** 1Kor 1:20; Za 24:7; Mdo 7:2; Yak 2:1
[t]**2:9** Isa 64:4; 65:17

"Hakuna jicho limepata kuona,
wala sikio limepata kusikia,
wala hayakuingia moyoni wowote,
yale Mungu amewaandalia
wale wampendao":

10 [a]Lakini mambo haya Mungu ametufunulia kwa Roho wake.

Roho huchunguza kila kitu, hata mambo ya ndani sana ya Mungu. 11 [b]Kwa maana ni nani anayejua mawazo ya mtu isipokuwa roho iliyo ndani ya huyo mtu? Vivyo hivyo hakuna mtu ajuaye mawazo ya Mungu isipokuwa Roho wa Mungu. 12 [c]Basi hatukupokea roho ya dunia bali Roho atokaye kwa Mungu, ili tuweze kuelewa kile kipawa ambacho Mungu ametupatia bure. 13 [d]Haya ndiyo tusemayo, si kwa maneno tuliyofundishwa kwa hekima ya wanadamu bali kwa maneno tuliyofundishwa na Roho, tukifafanua kweli za kiroho kwa maneno ya kiroho. 14 [e]Mtu ambaye hana Roho hawezi kupokea mambo yatokayo kwa Roho wa Mungu, kwa kuwa ni upuzi kwake, naye hawezi kuyaelewa kwa sababu hayo yanaeleweka tu kwa upambanuzi wa rohoni. 15 [f]Mtu wa kiroho hubainisha mambo yote, lakini yeye mwenyewe habainishwi na mtu yeyote.

16 [g]"Kwa maana ni nani aliyefahamu
mawazo ya Bwana
ili apate kumfundisha?"

Lakini sisi tunayo mawazo ya Kristo.

*Kuhusu Mgawanyiko Katika Kanisa*

3 [h]Ndugu zangu, mimi sikuweza kusema nanyi kama watu wa kiroho, bali kama watu wa mwilini, kama watoto wachanga katika Kristo. 2 [i]Naliwanywesha maziwa, wala si chakula kigumu, kwa kuwa hamkuwa tayari kwa hicho chakula. Naam, hata sasa hamko tayari. 3 [j]Ninyi bado ni watu wa mwilini. Kwa kuwa bado kuna wivu na magombano miongoni mwenu, je, ninyi si watu wa mwilini? Je, si mwaendelea kama watu wa kawaida? 4 [k]Kwa maana mmoja anaposema, "Mimi ni wa Paulo," na mwingine, "Mimi ni wa Apolo," je, ninyi si wanadamu wa kawaida?

5 [l]Kwani, Apolo ni nani? Naye Paulo ni nani? Ni watumishi tu ambao kupitia wao mliamini, kama vile Bwana alivyompa kila mtu huduma yake. 6 [m]Mimi nilipanda mbegu, Apolo akatia maji, lakini Mungu ndiye aliikuza. 7 [n]Hivyo mwenye kupanda na mwenye kutia maji si kitu, bali Mungu peke yake ambaye huifanya ikue. 8 [o]Apandaye mbegu ana lengo sawa na yule atiaye maji na kila mmoja atalipwa kulingana na kazi yake. 9 [p]Kwa kuwa sisi tu watendakazi pamoja na Mungu. Ninyi ni shamba la Mungu, jengo la Mungu.

10 [q]Kwa neema Mungu aliyonipa, niliweka msingi kama mjenzi stadi na mtu mwingine anajenga juu yake. Lakini kila mmoja inampasa awe mwangalifu jinsi anavyojenga. 11 [r]Kwa maana hakuna mtu yeyote awezaye kuweka msingi mwingine wowote isipokuwa ule uliokwisha kuwekwa, ambao ni Yesu Kristo. 12 Kama mtu yeyote akijenga juu ya msingi huu kwa kutumia dhahabu, fedha, vito vya thamani, miti, majani au nyasi, 13 [s]kazi yake itaonekana ilivyo, kwa kuwa Siku ile itaidhihirisha. Itadhihirishwa kwa moto, nao moto utapima ubora wa kazi ya kila mtu. 14 [t]Kama

[a]**2:10** Mt 13:11; 2Kor 12:1-7; Gal 1:12; 2:2; Efe 3:3-5; Yn 14:26
[b]**2:11** Yer 17:9; Mit 20:27
[c]**2:12** Rum 8:15; 1Kor 1:20-27; Yak 2:5
[d]**2:13** 1Kor 1:17
[e]**2:14** Yn 14:17; 1Kor 3:1
[f]**2:15** 1Kor 3:1; Gal 6:1
[g]**2:16** Isa 40:13; Rum 11:34; Yn 15:15
[h]**3:1** 1Kor 2:15; Rum 7:14; 1Kor 2:14; 14:20
[i]**3:2** Ebr 5:12-14; 1Pet 2:2; Yn 16:12
[j]**3:3** Rum 13:13; 1Kor 1:11; Gal 5:20
[k]**3:4** 1Kor 1:12
[l]**3:5** Mdo 18:24; 1Kor 4:1; 2Kor 6:4; Efe 3:7; Kol 1:23-25
[m]**3:6** Mdo 18:4-11; 1Kor 4:15; 9:1; 15:1
[n]**3:7** 2Kor 12:11; Gal 6:3
[o]**3:8** Za 18:20; 62:12; Mt 25:21; 1Kor 9:17
[p]**3:9** Mk 16:20; 2Kor 6:1; 1The 2:2; Isa 61:3; Efe 2:20-22; 1Pet 5:5
[q]**3:10** Rum 12:3; 15:20; Efe 2:20
[r]**3:11** Isa 28:16; Efe 2:20
[s]**3:13** 1Kor 4:5; 1:8; 2The 1:7-10; 2Tim 1:12-18; 4:8; Hes 31:22-23; Yer 23:28-29; Mal 3:3; 2The 1:7
[t]**3:14** 1Kor 3:8; 4:5

kile alichojenga kitabaki, atapokea thawabu
yake. 15 [a]Kama kazi kitateketea, atapata
hasara, ila yeye mwenyewe ataokolewa,
lakini tu kama mtu aliyenusurika kwenye
moto.
16 [b]Je, hamjui ya kwamba ninyi wenyewe
ni hekalu la Mungu na kwamba Roho wa
Mungu anakaa ndani yenu? 17 Kama mtu
yeyote akiliharibu hekalu la Mungu, Mungu
atamwangamiza; kwa maana hekalu la
Mungu ni takatifu, na ninyi ndiyo hilo
hekalu.
18 [c]Msijidanganye. Kama mtu yeyote
miongoni mwenu akidhani kuwa ana
hekima kwa viwango vya dunia hii,
inampasa awe mjinga ili apate kuwa
na hekima. 19 [d]Kwa maana hekima ya
ulimwengu huu ni upuzi mbele za Mungu.
Kama ilivyoandikwa: "Mungu huwanasa
wenye hekima katika hila yao," 20 [e]tena,
"Bwana anajua kwamba mawazo ya wenye
hekima ni ubatili." 21 [f]Hivyo basi, mtu
asijivune kuhusu wanadamu! Vitu vyote ni
vyenu, 22 [g]ikiwa ni Paulo au Apolo au Kefa[h]
au dunia au uzima au mauti, au wakati
uliopo au wakati ujao, haya yote ni yenu
23 [i]na ninyi ni wa Kristo, naye Kristo ni wa
Mungu.

### *Mawakili Wa Siri Za Mungu*

4 [j]Basi, watu na watuhesabu sisi kuwa tu
watumishi wa Kristo na mawakili wa siri
za Mungu. 2 [k]Tena, litakiwalo ni mawakili
waonekane kuwa waaminifu. 3 Lakini
kwangu mimi ni jambo dogo sana kwamba
nihukumiwe na ninyi au na mahakama
yoyote ya kibinadamu. Naam, hata mimi
mwenyewe sijihukumu. 4 [l]Dhamiri yangu ni
safi, lakini hilo halinihesabii kuwa asiye na
hatia. Bwana ndiye anihukumuye. 5 [m]Kwa
hiyo msihukumu jambo lolote kabla ya
wakati wake. Ngojeni mpaka Bwana
atakapokuja. Yeye atayaleta nuruni mambo
yale yaliyofichwa gizani, na kuweka wazi
nia za mioyo ya wanadamu. Wakati huo
kila mmoja atapokea sifa anayostahili
kutoka kwa Mungu.
6 [n]Basi ndugu zangu, mambo haya
nimeyafanya kwangu binafsi na Apolo kwa
faida yenu, ili mweze kujifunza kutoka kwetu
maana ya ule usemi usemao, "Msivuke zaidi
ya yale yaliyoandikwa." Hivyo hamtajivunia
mtu fulani na kumdharau mwingine. 7 [o]Kwa
maana ni nani aliyewafanya kuwa tofauti
na wengine? Ni nini mlicho nacho ambacho
hamkupokea? Nanyi kama mlipokea, kwa
nini mnajivuna kama vile hamkupokea?
8 [p]Sasa tayari mnayo yale yote
mnayohitaji! Tayari mmekwisha kuwa
matajiri! Mmekuwa wafalme, tena bila
sisi! Laiti mngekuwa wafalme kweli ili na
sisi tupate kuwa wafalme pamoja nanyi!
9 [q]Kwa maana ninaona kwamba Mungu
ametuweka sisi mitume katika nafasi ya
mwisho kabisa, kama watu waliohukumiwa
kufa kwenye uwanja wa tamasha, kwa
sababu tumefanywa kuwa maonyesho
kwa ulimwengu wote, kwa malaika na
kwa wanadamu pia. 10 [r]Kwa ajili ya Kristo
sisi ni wajinga, lakini ninyi mna hekima
sana ndani ya Kristo. Sisi tu dhaifu, lakini
ninyi mna nguvu. Tunadharauliwa, lakini
ninyi mnaheshimiwa. 11 [s]Mpaka saa hii tuna
njaa na kiu, tu uchi, tumepigwa na hatuna
makao. 12 [t]Tunafanya kazi kwa bidii kwa
mikono yetu wenyewe. Tunapolaaniwa,
tunabariki, tunapoteswa, tunastahimili,

[a]**3:15** Yud 23
[b]**3:16** 1Kor 6:9; 2Kor 6:16; Efe 2:21-22; Ebr 3:6; Rum 8:9
[c]**3:18** Isa 5:12; 1Kor 8:2; Gal 6:3; 1Kor 1:20
[d]**3:19** Rum 1:22; 1Kor 1:20-27; Ay 5:13
[e]**3:20** Za 94:11
[f]**3:21** 1Kor 4:6; Rum 8:32
[g]**3:22** 1Kor 1:12; Rum 8:38
[h]22 Yaani Petro.
[i]**3:23** 1Kor 15:23; 2Kor 10:7; Gal 3:29
[j]**4:1** 1Kor 3:5; 9:17; Tit 1:7; Rum 16:25
[k]**4:2** Lk 12:42
[l]**4:4** Mdo 23:1; Rum 2:13; 2Kor 10:18
[m]**4:5** Mt 7:12; 1The 2:19; Ay 12:22; Za 90:8; 1Kor 3:13; Rum 2:29
[n]**4:6** 1Kor 1:19-31; 3:19-20; 1:21
[o]**4:7** Yn 3:27; Rum 12:3-6
[p]**4:8** Ufu 3:17-18
[q]**4:9** Rum 8:36; Za 71:7; Ebr 10:33
[r]**4:10** 1Kor 1:18; Mdo 17:18; 26:24; 1Kor 3:18; 2Kor 11:19; 1Kor 2:3
[s]**4:11** Rum 8:35; 2Kor 11:23-27
[t]**4:12** Mdo 18:3; Rum 12:14; 1Pet 3:4; Mt 5:44

13 [a]tunaposingiziwa, tunajibu kwa upole.
Mpaka sasa tumekuwa kama takataka ya
dunia na uchafu wa ulimwengu.
14 [b]Siwaandikii mambo haya ili
kuwaaibisha, bali ili kuwaonya, kama
wanangu wapendwa. 15 [c]Hata kama mnao
walimu 10,000 katika Kristo, lakini hamna
baba wengi. Mimi nilikuwa baba yenu
katika Kristo Yesu kwa kuwaletea Injili.
16 [d]Basi nawasihi igeni mfano wangu.
17 [e]Kwa sababu hii ninamtuma Timotheo,
mwanangu mpendwa na mwaminifu katika
Bwana. Yeye atawakumbusha kuhusu
njia za maisha yangu katika Kristo Yesu,
ambayo yanakubaliana na mafundisho
yangu ninayofundisha katika kila kanisa.
18 [f]Baadhi yenu mmekuwa na jeuri
mkidhani kuwa sitafika kwenu. 19 [g]Lakini
kama Bwana akipenda, nitafika kwenu
mapema, nami nitapenda kujua, si tu kile
wanachosema hawa watu jeuri, bali pia
kujua nguvu yao. 20 [h]Kwa kuwa Ufalme wa
Mungu si maneno matupu tu bali ni nguvu.
21 [i]Ninyi amueni. Je, nije kwenu na fimbo,
au nije kwa upendo na kwa roho ya upole?

*Mwasherati Atengwe*

5 [j]Yamkini habari imeenea ya kuwa
miongoni mwenu kuna uzinzi ambao
haujatokea hata miongoni mwa watu
wasiomjua Mungu: Kwamba mtu anaishi
na mke wa baba yake. 2 [k]Nanyi mwajivuna!
Je, haiwapasi kuhuzunika na kumtenga
na ushirika wenu mtu huyo aliyefanya
mambo hayo? 3 [l]Hata kama siko pamoja
nanyi katika mwili, niko nanyi katika
roho. Nami nimekwisha kumhukumu mtu
huyo aliyetenda jambo hili, kama vile
ningekuwepo. 4 [m]Mnapokutana katika Jina
la Bwana wetu Yesu nami nikiwepo pamoja
nanyi katika roho na uweza wa Bwana Yesu
ukiwepo, 5 [n]mkabidhini mtu huyu kwa
Shetani, ili mwili wake uharibiwe, ili roho
yake iokolewe katika siku ya Bwana.
6 [o]Majivuno yenu si mazuri. Je, hamjui
ya kwamba chachu kidogo huchachusha
donge zima la unga? 7 [p]Ondoeni chachu ya
kale ili mpate kuwa donge jipya lisilotiwa
chachu, kama vile mlivyo. Kwa maana
Kristo, Mwana-Kondoo wetu wa Pasaka
amekwisha tolewa kuwa dhabihu. 8 [q]Kwa
hiyo, tusiiadhimishe sikukuu hii, kwa
chachu ya zamani, chachu ya nia mbaya
na uovu, bali kwa mkate usiotiwa chachu,
ndio weupe wa moyo na kweli.
9 [r]Niliwaandikia katika waraka wangu
kuwa msishirikiane na wazinzi. 10 [s]Sina
maana kwamba msishirikiane na wazinzi
wa ulimwengu huu, au wenye tamaa
mbaya, wanyang'anyi au waabudu
sanamu. Kwa kufanya hivyo ingewalazimu
mtoke ulimwenguni humu. 11 [t]Lakini sasa
nawaandikia kwamba msishirikiane na
mtu yeyote anayejiita ndugu, hali akiwa
ni mzinzi, au mwenye tamaa mbaya,
mwabudu sanamu au msingiziaji, mlevi au
mdhalimu. Mtu kama huyo hata msile naye.
12 [u]Yanihusu nini kuwahukumu wale
watu walio nje ya kanisa? Je, si mnapaswa
kuwahukumu hao walio ndani? 13 [v]Mungu
atawahukumu hao walio nje. "Ninyi
mwondoeni huyo mtu mwovu miongoni
mwenu."

[a]**4:13** Yer 20:18; Mao 3:45; Kum 17:7; 22:24
[b]**4:14** 1Kor 6:5; 15:34; 2The 3:14; 1The 2:11
[c]**4:15** 1Kor 9:12-23; 15:1
[d]**4:16** 1Kor 11:1; Flp 3:17; 4:9; 1The 1:6; 2The 3:7-9
[e]**4:17** 1Kor 16:10; Mdo 16:1; 1Tim 1:2
[f]**4:18** Yer 43:2
[g]**4:19** 1Kor 16:5-6; 2Kor 1:15; Mdo 18:21
[h]**4:20** Rum 14:17; 15:13
[i]**4:21** 2Kor 1:23; 2:1; 13:2-10
[j]**5:1** Law 18:8; Kum 22:30; 27:20
[k]**5:2** 2Kor 7:7-11
[l]**5:3** Kol 2:5; 1The 2:17
[m]**5:4** 2The 3:6
[n]**5:5** 1Tim 1:20; Mt 4:10; 1Kor 1:8
[o]**5:6** Yak 4:16; Mt 16:6-12; Gal 5:6
[p]**5:7** Kut 12:3-21; Mk 14:12; 1Pet 1:19
[q]**5:8** Law 18:8; Kum 22:30; 27:20
[r]**5:9** Kut 12:45; Kum 16:3
[s]**5:10** Efe 5:11; 2The 3:6-14
[t]**5:11** 1Kor 10:27
[u]**5:12** Rum 7:1; 1Kor 10:7-14; Rum 16:17
[v]**5:13** Mk 4:11; 1Kor 6:14; Kum 13:5; 17:7; 19:19; 22:21; 24; 24:7; Amu 20:13

*Kushtakiana Miongoni Mwa Waumini*

6 [a]Kama mtu yeyote wa kwenu ana ugomvi
na mwenzake, anathubutuje kuupeleka
kwa wasiomcha Mungu ili kuamuliwa
badala ya kuupeleka kwa watakatifu? 2 [b]Je,
hamjui kwamba watakatifu watauhukumu
ulimwengu? Nanyi kama mtauhukumu
ulimwengu, je, hamwezi kuamua mambo
madogo madogo? 3 [c]Hamjui kwamba
tutawahukumu malaika? Je, si zaidi mambo
ya maisha haya? 4 [d]Kwa hiyo kama kuna
ugomvi miongoni mwenu kuhusu mambo
kama haya, chagueni kuwa waamuzi, watu
ambao wanaonekana hata sio wa heshima
katika kanisa. 5 [e]Nasema hivi ili mwone
aibu. Je, inawezekana kuwa miongoni
mwenu hakuna mtu mwenye hekima ya
kutosha kuamua ugomvi kati ya waaminio?
6 [f]Badala yake ndugu mmoja anampeleka
mwenzake mahakamani, tena mbele ya
watu wasioamini!

7 [g]Huko kuwa na mashtaka miongoni
mwenu ina maana kwamba tayari ni
kushindwa kabisa. Kwa nini msikubali
kutendewa mabaya? Kwa nini msikubali
kunyang'anywa? 8 [h]Badala yake, ninyi
wenyewe mwadanganya na kutenda
mabaya, tena mwawatendea ndugu zenu.

9 [i]Je, hamjui kwamba wasio haki
hawataurithi Ufalme wa Mungu?
Msidanganyike: Waasherati, wala waabudu
sanamu, wala wazinzi, wala wahanithi, wala
walawiti, 10 [j]wala wezi, wala wenye tamaa
mbaya, wala walevi, wala wanaodhihaki,
wala wanyang'anyi hawataurithi Ufalme wa
Mungu. 11 [k]Baadhi yenu mlikuwa kama hao.
Lakini mlioshwa, mlitakaswa, mlihesabiwa
haki kwa jina la Bwana Yesu Kristo na
katika Roho wa Mungu wetu.

*Dhambi Za Zinaa*

12 [l]"Vitu vyote ni halali kwangu": lakini
si vitu vyote vyenye faida. "Vitu vyote
ni halali kwangu": lakini sitatawaliwa
na kitu chochote. 13 [m]"Chakula ni cha
tumbo, na tumbo ni la chakula": lakini
Mungu ataviangamiza vyote viwili. Mwili
haukuumbwa kwa ajili ya zinaa bali kwa
ajili ya Bwana na Bwana kwa ajili ya
mwili. 14 [n]Naye Mungu aliyemfufua Bwana
kutoka kwa wafu atatufufua sisi pia kwa
uweza wake. 15 [o]Je, hamjui kwamba miili
yenu ni viungo vya Kristo mwenyewe? Je,
nichukue viungo vya mwili wa Kristo na
kuviunganisha na mwili wa kahaba? La
hasha! 16 [p]Hamjui kwamba aliyeungwa na
kahaba anakuwa mwili mmoja naye? Kwa
kuwa imenenwa, "Hao wawili watakuwa
mwili mmoja." 17 [q]Lakini mtu aliyeungwa
na Bwana anakuwa roho moja naye.

18 [r]Ikimbieni zinaa. Dhambi zingine zote
atendazo mtu ziko nje ya mwili wake,
lakini yeye aziniye hutenda dhambi ndani
ya mwili wake mwenyewe. 19 [s]Je, hamjui
ya kwamba miili yenu ni hekalu la Roho
Mtakatifu akaaye ndani yenu, ambaye
mmepewa na Mungu? Ninyi si mali yenu
wenyewe, 20 [t]kwa maana mmenunuliwa
kwa gharama. Kwa hiyo mtukuzeni Mungu
katika miili yenu.

*Kuhusu Ndoa*

7 [u]Basi kuhusu mambo yale mliyoyaandika:
Ni vyema mwanaume asimguse
mwanamke. 2 Lakini ili kuepuka zinaa, kila

---

[a]**6:1** Mt 18:7
[b]**6:2** Mt 19:28; Lk 22:30; 1Kor 5:12
[c]**6:3** 1Kor 4:14; Mdo 1:15
[d]**6:4** 1Kor 5:12
[e]**6:5** 1Kor 4:14; Mdo 1:15
[f]**6:6** Rum 7:1; 2Kor 6:14-15; 1Tim 5:8
[g]**6:7** Mt 5:39-40; 1The 5:15; 1Pet 3:9
[h]**6:8** 1The 4:6; Kum 17:7; 19; 19; 21:21; 22:21, 24; 24:7
[i]**6:9** Mt 25:34; Ay 13:9; 1Kor 15:33; Gal 6:7; Yak 1:16; Law 18:20; Kum 22:22; Law 18:22
[j]**6:10** 1Tim 1:10; Ufu 21:8; 22:15
[k]**6:11** Efe 2:2; Mdo 22:16; 1Kor 1:2; Rum 12:1
[l]**6:12** 1Kor 10:23
[m]**6:13** Kol 2:22; Rum 12:1
[n]**6:14** Mdo 2:24; Rum 6:5; Efe 1:19-20; 1The 4:16
[o]**6:15** Rum 12:5
[p]**6:16** Mwa 2:24; Mt 19:5; Efe 5:31
[q]**6:17** Yn 17:21-23; Rum 8:8-11; Gal 2:20
[r]**6:18** 1Kor 5:1; 2Kor 12:21; Gal 5:19; Efe 5:3; 1The 4:3-4; Ebr 13:4; Rum 6:12
[s]**6:19** Yn 2:21; Rum 14:7-8
[t]**6:20** Za 74:2; Mt 20:28; Mdo 20:28; 1Kor 7:23; Ufu 5:9; 14:4; Flp 1:20
[u]**7:1** 1Kor 7:8, 26

mwanaume na awe na mke wake mwenyewe
na kila mwanamke awe na mume wake
mwenyewe. 3 [a]Mume atimize wajibu
wake wa ndoa kwa mkewe, naye vivyo
hivyo mke kwa mumewe. 4 Mwanamke
hana mamlaka juu ya mwili wake bali
mumewe, wala mume hana mamlaka juu
ya mwili wake bali mkewe. 5 [b]Msinyimane,
isipokuwa mmekubaliana kufanya hivyo
kwa muda fulani ili mweze kujitoa kwa
maombi, kisha mrudiane tena ili Shetani
asije akapata nafasi ya kuwajaribu kwa
sababu ya kutokuwa na kiasi. 6 [c]Nasema
haya kama ushauri na si amri. 7 [d]Laiti watu
wangekuwa kama mimi nilivyo. Lakini kila
mtu amepewa kipawa chake kutoka kwa
Mungu, mmoja ana kipawa cha namna hii
na mwingine ana cha namna ile.

8 [e]Kwa wale wasiooa na kwa wajane,
nasema hivi, ingekuwa vizuri wasioe.
9 [f]Lakini kama hawawezi kujizuia, basi
waoe na kuolewa, kwa maana ni afadhali
kuoa au kuolewa kuliko kuwaka tamaa.

10 [g]Kwa wale waliooana nawapa amri
(si mimi ila ni Bwana): Mke asitengane na
mumewe. 11 [h]Lakini akitengana, ni lazima
akae bila kuolewa, ama sivyo apatane tena
na mumewe. Wala mume asimpe mkewe
talaka.

12 [i]Lakini kwa wengine nasema (si
Bwana ila ni mimi): Kama ndugu ana mke
asiyeamini, naye huyo mke anakubali kuishi
pamoja naye, basi asimwache. 13 Naye
mwanamke aaminiye kama ameolewa na
mwanaume asiyeamini na huyo mume
anakubali kuishi naye, basi huyo mwanamke
asimwache. 14 [j]Kwa maana huyo mume
asiyeamini anatakaswa kupitia mkewe,
naye mke asiyeamini anatakaswa kupitia
mumewe anayeamini. Kama isingalikuwa
hivyo watoto wenu wangalikuwa si safi,
lakini ilivyo sasa wao ni watakatifu.
15 [k]Lakini kama yule asiyeamini akijitenga,
basi afanye hivyo. Katika hali kama hiyo
mwanamke au mwanaume aaminiye
hafungwi, kwa sababu Mungu ametuita
tuishi kwa amani. 16 [l]Wewe mke, unajuaje
kama utamwokoa mumeo? Au wewe mume
unajuaje kama utamwokoa mkeo?

### *Kuishi Kama Alivyoagiza Bwana*

17 [m]Lakini kila mtu na aishi maisha
aliyopangiwa na Bwana, yale Mungu
aliyomwitia. Hii ni sheria ninayoiweka
kwa makanisa yote. 18 [n]Je, mtu alikuwa
tayari ametahiriwa alipoitwa? Asijifanye
asiyetahiriwa. Je, mtu alikuwa hajatahiriwa
alipoitwa? Asitahiriwe. 19 [o]Kutahiriwa si
kitu, na kutokutahiriwa si kitu. Lakini
kuzitii amri za Mungu ndilo jambo muhimu.
20 [p]Basi kila mmoja wenu na abaki katika
hali aliyoitwa nayo. 21 Je, wewe ulipoitwa
ulikuwa mtumwa? Jambo hilo lisikusumbue.
Ingawaje unaweza kupata uhuru, tumia
nafasi uliyo nayo sasa kuliko wakati
mwingine wowote. 22 [q]Kwa maana yeyote
aliyeitwa katika Bwana akiwa mtumwa
yeye ni mtu huru kwa Bwana, kama vile
yeyote aliyekuwa huru alipoitwa yeye ni
mtumwa wa Kristo. 23 [r]Mlinunuliwa kwa
gharama; msiwe watumwa wa wanadamu.
24 Ndugu zangu, kama kila mtu alivyoitwa,
akae katika wito wake alioitiwa na Mungu.

### *Wajane Na Wasioolewa*

25 [s]Basi, kuhusu wale walio bikira,
mimi sina amri kutoka kwa Bwana, lakini
mimi natoa shauri kama mtu ambaye
ni mwaminifu kwa rehema za Bwana.

---

[a]**7:3** Kut 21:10; 1Pet 3:7
[b]**7:5** Kut 19:15; 1Sam 21:4-5; Mt 4:10; 1The 3:5
[c]**7:6** 2Kor 8:8
[d]**7:7** 1Kor 9:5; Mt 19:11-12; Rum 12:6; 1Kor 12:4-11
[e]**7:8** 1Kor 7:1, 26
[f]**7:9** 1Tim 5:14
[g]**7:10** Mal 2:14-16; Lk 16:18
[h]**7:11** Rum 7:2-3
[i]**7:12** 2Kor 11:17
[j]**7:14** Mk 2:15
[k]**7:15** Rum 14:19; 1Kor 14:19; 14:33
[l]**7:16** Rum 11:16; 1Pet 3:1
[m]**7:17** Rum 12:3; 1Kor 4:17; 14:33; 2Kor 8:18; 11:28
[n]**7:18** Mdo 15:1-2; 15:19, 24; 28; Gal 5:2
[o]**7:19** Rum 2:25-27; Gal 5:6; 6:15; Kol 3:11
[p]**7:20** 1Kor 7:24
[q]**7:22** Yn 8:32-36; Rum 6:22
[r]**7:23** 1Kor 6:20; 1Pet 1:18, 19; Law 25:42
[s]**7:25** 2Kor 8:8; 4:1; 1Tim 1:13-16

26 [a]Kwa sababu ya shida iliyoko kwa sasa,
naona ni vyema mkibaki kama mlivyo.
27 Je, umeolewa? Basi usitake talaka. Je,
hujaoa? Usitafute mke. 28 [b]Lakini kama
ukioa, hujatenda dhambi; na kama bikira
akiolewa, hajatenda dhambi. Lakini wale
wanaooa watakabiliana na matatizo
mengi katika maisha haya, nami nataka
kuwazuilia hayo.

29 [c]Lakini ndugu zangu, nina maana
kwamba muda uliobaki ni mfupi. Tangu
sasa wale waliooa waishi kama wasio
na wake; 30 nao wanaoomboleza, kama
ambao hawaombolezi; wenye furaha kama
wasiokuwa nayo; wale wanaonunua, kama
vile vitu walivyonunua si mali yao; 31 [d]nao
wale wanaoshughulika na vitu vya dunia
hii, kama ambao hawahusiki navyo. Kwa
maana dunia hii kama tunavyoiona sasa
inapita.

32 [e]Ningetaka msiwe na masumbufu.
Mwanaume ambaye hajaoa anajishughulisha
na mambo ya Bwana, jinsi ya kumpendeza
Bwana. 33 [f]Lakini mwanaume aliyeoa
anajishughulisha na mambo ya dunia, jinsi
ya kumfurahisha mkewe, 34 [g]na mawazo yake
yamegawanyika. Mwanamke asiyeolewa
hujishughulisha na mambo ya Bwana: lengo
lake ni awe mtakatifu kimwili na kiroho.
Lakini yule aliyeolewa hujishughulisha
na mambo ya dunia, jinsi atakavyoweza
kumfurahisha mumewe. 35 [h]Ninasema haya
kwa faida yenu wenyewe, sio ili kuwawekea
vizuizi bali mpate kuishi kwa jinsi ilivyo
vyema bila kuvutwa pengine katika kujitoa
kwenu kwa Bwana.

36 [i]Kama mtu yeyote anadhani kwamba
hamtendei ilivyo sawa mwanamwali
ambaye amemposa, naye akiwa umri
wake unazidi kuendelea na mtu huyo
anajisikia kwamba inampasa kuoa, afanye
kama atakavyo. Yeye hatendi dhambi.
Yawapasa waoane. 37 Lakini mwanaume
ambaye ameamua moyoni mwake kutooa
bila kulazimishwa na mtu yeyote, bali
anaweza kuzitawala tamaa zake kutomwoa
huyo mwanamwali, basi anafanya ipasavyo.
38 [j]Hivyo basi, mwanaume amwoaye
mwanamwali afanya vyema, lakini yeye
asiyemwoa afanya vyema zaidi.

39 [k]Mwanamke aliyeolewa amefungwa na
sheria maadamu mumewe yu hai. Lakini
mumewe akifa, basi mwanamke huyo
yuko huru kuolewa na mume mwingine
ampendaye, lakini lazima awe katika
Bwana. 40 [l]Lakini kwa maoni yangu,
angekuwa na furaha zaidi akibaki alivyo.
Nami nadhani pia nina Roho wa Mungu.

### *Chakula Kilichotolewa Sadaka Kwa Sanamu*

8 [m]Sasa kuhusu chakula kilichotolewa
sadaka kwa sanamu, tunajua kwamba
“sisi sote tuna ujuzi.” Lakini ujuzi hujivuna,
bali upendo hujenga. 2 [n]Mtu yeyote
anayedhani kwamba anajua kitu, bado
hajui kama impasavyo kujua. 3 [o]Lakini
mtu ampendaye Mungu, hujulikana naye
Mungu.

4 [p]Hivyo basi, kuhusu kula chakula
kilichotolewa sadaka kwa sanamu: Tunajua
kwamba “Sanamu si kitu chochote kabisa
duniani,” na kwamba “Kuna Mungu
mmoja tu.” 5 [q]Kwa kuwa hata kama wapo
hao wanaoitwa miungu, kama wakiwa
mbinguni au duniani (kama ilivyo kweli
wapo “miungu” wengi na “mabwana”
wengi), 6 [r]kwetu sisi yuko Mungu mmoja,
aliye Baba, ambaye vitu vyote vyatoka
kwake na kwa ajili yake sisi twaishi; na
kuna Bwana mmoja tu, Yesu Kristo, ambaye

---

[a]**7:26** 1Kor 7:1, 8
[b]**7:28** 1Kor 7:36
[c]**7:29** Rum 13:11-12
[d]**7:31** Ebr 12:27
[e]**7:32** 1Tim 5:5
[f]**7:33** Lk 14:20; Efe 5:29
[g]**7:34** Lk 2:37
[h]**7:35** Za 86:11
[i]**7:36** 1Kor 7:28
[j]**7:38** Ebr 13:4
[k]**7:39** Rum 7:2-3; 2Kor 6:14
[l]**7:40** 1Kor 7:28
[m]**8:1** Mdo 15:20; Rum 15:14
[n]**8:2** 1Kor 3:8-12; 1Tim 6:4
[o]**8:3** Yer 1:5; Rum 8:29; Gal 4:9
[p]**8:4** Kut 34:15; Mdo 14:15; 1Kor 10:19; Gal 4:8; Kum 6:4; Za 86:10; Efe 4:6; 1Tim 2:5
[q]**8:5** 2The 2:4; Za 82:6; Yn 10:34
[r]**8:6** Mal 2:10; Rum 11:36; Efe 4:5; Yn 1:3

kwa yeye vitu vyote vimekuwepo na kwa
yeye tunaishi.
7 [a]Lakini si wote wanaojua jambo hili.
Baadhi ya watu bado wamezoea sanamu
kuwa halisi hivi kwamba wanapokula
chakula kama hicho wanadhani kimetolewa
sadaka kwa sanamu na kwa kuwa dhamiri
zao ni dhaifu, dhamiri yao inanajisika.
8 [b]Lakini chakula hakituleti karibu
na Mungu, wala hatupotezi chochote
tusipokula, wala hatuongezi chochote kama
tukila.
9 [c]Lakini angalieni jinsi mnavyotumia
uhuru wenu usije ukawa kikwazo kwao
walio dhaifu. 10 [d]Kwa maana kama mtu
yeyote mwenye dhamiri dhaifu akiwaona
ninyi wenye ujuzi huu mkila katika hekalu
la sanamu, je, si atatiwa moyo kula chakula
kilichotolewa sadaka kwa sanamu? 11 [e]Kwa
njia hiyo, huyo ndugu mwenye dhamiri
dhaifu, ambaye Kristo alikufa kwa ajili yake,
ataangamia kwa sababu ya ujuzi wenu.
12 [f]Mnapotenda dhambi dhidi ya ndugu zenu
kwa njia hii na kujeruhi dhamiri zao zilizo
dhaifu, mnamkosea Kristo. 13 [g]Kwa hiyo,
kama kile ninachokula kitamfanya ndugu
yangu aanguke katika dhambi, sitakula
nyama kamwe, nisije nikamfanya ndugu
yangu aanguke.

*Haki Za Mtume*

9 [h]Je, mimi si huru? Je, mimi si mtume?
Je, mimi sikumwona Yesu, Bwana wetu?
Je, ninyi si matunda ya kazi yangu katika
Bwana? 2 [i]Hata kama mimi si mtume kwa
wengine, hakika mimi ni mtume kwenu,
kwa maana ninyi ni mhuri wa utume wangu
katika Bwana.
3 Huu ndio utetezi wangu kwa hao
wanaokaa kunihukumu. 4 [j]Je, hatuna haki
ya kula na kunywa? 5 [k]Je, hatuna haki
ya kusafiri na mke anayeamini, kama
wanavyofanya mitume wengine na ndugu
zake Bwana na Kefa?[l] 6 [m]Au ni mimi na
Barnaba tu inatubidi kufanya kazi ili tuweze
kupata mahitaji yetu?
7 [n]Ni askari yupi aendaye vitani kwa
gharama zake mwenyewe? Ni nani
apandaye shamba la mizabibu na asile
matunda yake? Ni nani achungaye
kundi na asipate maziwa yake. 8 Je,
nasema mambo haya katika mtazamo
wa kibinadamu tu? Je, sheria haisemi
vivyo hivyo? 9 [o]Kwa maana imeandikwa
katika Sheria ya Mose: "Usimfunge maksai
kinywa apurapo nafaka." Je, Mungu hapa
anahusika na ng'ombe? 10 [p]Je, Mungu
hasemi haya hasa kwa ajili yetu? Hakika
yameandikwa kwa ajili yetu, kwa sababu
mtu anapolima na mpuraji akapura nafaka,
wote wanapaswa kufanya hivyo wakiwa na
tumaini la kushiriki mavuno. 11 [q]Je, ikiwa
sisi tulipanda mbegu ya kiroho miongoni
mwenu, itakuwa ni jambo kubwa iwapo
tutavuna vitu vya mwili kutoka kwenu?
12 [r]Kama wengine wana haki ya kupata
msaada kutoka kwenu, isingepasa tuwe
na haki hiyo hata zaidi?
Lakini sisi hatukutumia haki hii. Kinyume
chake, tunavumilia kila kitu ili tusije
tukazuia Injili ya Kristo. 13 [s]Je, hamjui
kwamba, watu wafanyao kazi hekaluni
hupata chakula chao kutoka hekaluni,
nao wale wahudumiao madhabahuni
hushiriki kile kitolewacho madhabahuni?
14 [t]Vivyo hivyo, Bwana ameamuru kwamba

---

[a]**8:7** Rum 14:14; 1Kor 10:28
[b]**8:8** Rum 14:17
[c]**8:9** 2Kor 6:3; Gal 5:13; Rum 14:1
[d]**8:10** 1Kor 8:1, 4, 7; 10:28, 32
[e]**8:11** Rum 14:15-20
[f]**8:12** Mt 18:6; 25:40-45
[g]**8:13** Mt 5:29; Rum 14:21; 2Kor 11:29
[h]**9:1** 1Kor 1:1; 2Kor 12:12; 1Kor 15:8; 3:6; 4:15
[i]**9:2** 2Kor 3:2-3; 1Kor 12:12
[j]**9:4** Mdo 18:3; Lk 10:8; 1Kor 9:14
[k]**9:5** 1Kor 7:7-8; Mt 12:46; 1Kor 1:12
[l]5 Yaani Petro.
[m]**9:6** Mdo 4:36; 2The 3:8, 9
[n]**9:7** 2Tim 2:3-4; Kum 20:6; Mit 27:18; 1Kor 3:6-8
[o]**9:9** Kum 25:4; 1Tim 5:18; Kum 22:1-4; Mit 12:10
[p]**9:10** Rum 4:23-24; Mit 11:25; 2Tim 2:6
[q]**9:11** Rum 15:27; Gal 6:6
[r]**9:12** Mdo 18:3; 2Kor 6:3; 11:7-12
[s]**9:13** Law 6:16-26; Kum 18:1
[t]**9:14** 1Tim 5:18; Mt 10:10; Lk 10:7; Gal 6:6; 1Tim 5:17

wale wanaohubiri Injili wapate riziki yao
kutokana na Injili.
15 [a]Lakini sijatumia hata mojawapo ya
haki hizi. Nami siandiki haya nikitumaini
kwamba mtanifanyia mambo hayo. Heri
nife kuliko mtu yeyote kuninyima huku
kujisifu kwangu. 16 [b]Lakini ninapohubiri
Injili siwezi kujisifu maana ninalazimika
kuhubiri. Ole wangu nisipoihubiri Injili!
17 [c]Nikihubiri kwa hiari, ninayo thawabu.
Lakini kama si kwa hiari, basi ninachofanya
ni kutekeleza tu uwakili niliowekewa.
18 [d]Basi je, thawabu yangu ni nini? Thawabu
yangu ni hii: Ya kwamba katika kuhubiri
Injili niitoe bila gharama, bila kutumia kwa
utimilifu uwezo wangu nilio nao katika
Injili.
19 [e]Ingawa mimi ni huru, wala si mtumwa
wa mtu yeyote, nimejifanya kuwa mtumwa
wa kila mtu, ili niweze kuwavuta wengi
kadri iwezekanavyo. 20 [f]Kwa Wayahudi,
nilikuwa kama Myahudi, ili niwapate
Wayahudi. Kwa watu wale walio chini
ya sheria, nilikuwa kama aliye chini ya
sheria (ingawa mimi siko chini ya sheria),
ili niweze kuwapata wale walio chini
ya sheria. 21 [g]Kwa watu wasio na sheria
nilikuwa kama asiye na sheria (ingawa
siko huru mbali na sheria ya Mungu, bali
niko chini ya sheria ya Kristo), ili niweze
kuwapata wale wasio na sheria. 22 [h]Kwa
walio dhaifu nilikuwa dhaifu, ili niweze
kuwapata walio dhaifu. Nimekuwa mtu wa
hali zote kwa watu wote ili kwa njia yoyote
niweze kuwaokoa baadhi yao. 23 Nafanya
haya yote kwa ajili ya Injili, ili nipate
kushiriki baraka zake.
24 [i]Je, hamjui kwamba katika mashindano
ya mbio wote wanaoshindana hukimbia,
lakini ni mmoja wao tu apewaye tuzo? Kwa
hiyo kimbieni katika mashindano kwa jinsi
ambavyo mtapata tuzo.
25 [j]Kila mmoja anayeshiriki katika
mashindano hufanya mazoezi makali. Wao
hufanya hivyo ili wapokee taji isiyodumu,
lakini sisi tunafanya hivyo ili kupata taji
idumuyo milele. 26 [k]Kwa hiyo mimi sikimbii
kama mtu akimbiaye bila lengo, sipigani
kama mtu anayepiga hewa, 27 [l]la, bali
nautesa mwili wangu na kuutumikisha ili
nikiisha kuwahubiria wengine, mimi nisiwe
mtu wa kukataliwa.

*Onyo Kutoka Historia Ya Waisraeli*

10 [m]Ndugu zangu, sitaki mkose kufahamu
ukweli huu kwamba baba zetu
walikuwa wote chini ya wingu na kwamba
wote walipita katikati ya bahari. 2 [n]Wote
wakabatizwa kuwa wa Mose ndani ya
lile wingu na ndani ya ile bahari. 3 [o]Wote
walikula chakula kile kile cha roho, 4 [p]na
wote wakanywa kile kile kinywaji cha
roho, kwa maana walikunywa kutoka ule
mwamba wa roho uliofuatana nao, nao ule
mwamba ulikuwa Kristo. 5 [q]Lakini Mungu
hakupendezwa na wengi wao, kwa hiyo
miili yao ilitapakaa jangwani.
6 [r]Basi mambo haya yalitokea kama
mifano ili kutuzuia tusiweke mioyo
yetu katika mambo maovu kama wao
walivyofanya. 7 [s]Msiwe waabudu sanamu,
kama baadhi yao walivyokuwa, kama
ilivyoandikwa, "Watu waliketi chini kula
na kunywa, kisha wakainuka kucheza na
kufanya sherehe za kipagani." 8 [t]Wala

[a]**9:15** Mdo 18:3; 2Kor 11:9-10
[b]**9:16** Rum 1:14; Mdo 9:15; 26:15-18
[c]**9:17** 1Kor 3:8-14; 4:1; Gal 2:7; Kol 1:25
[d]**9:18** 2Kor 11:7; 12:13; 1Kor 10:33; 2Kor 4:5; 1Kor 7:31
[e]**9:19** 2Kor 4:5; Gal 5:13; Mt 18:15; 1Pet 3:1
[f]**9:20** Mdo 16:3; 21:20-26; Rum 11:14; 2:12
[g]**9:21** Rum 2:12-14; Gal 6:2
[h]**9:22** Rum 14:1; 1Kor 2:3; 10:33; Rum 11:14
[i]**9:24** Flp 3:14; Kol 2:18; Gal 2:2; 5:7; Flp 2:16; 2Tim 4:7; Ebr 12:1
[j]**9:25** 2Tim 2:5; 4:8; Yak 1:12; 1Pet 5:4; Ufu 2:10; 3:11
[k]**9:26** 1Tim 6:12; 2Kor 2:5; 1Kor 9:24
[l]**9:27** Rum 8:12; 8:13; Kol 3:5; Rum 6:18-19; Yer 6:30; 2Kor 13:5, 6; Lk 10:7
[m]**10:1** Rum 11:25; Kut 13:21; Za 105:39; Kut 14:22-29; Za 66:6
[n]**10:2** Rum 6:3
[o]**10:3** Yn 6:31; Kut 16:15, 35; Neh 9:15, 20; Za 78:24
[p]**10:4** Kut 17:6; Hes 20:11; Za 78:15
[q]**10:5** Hes 14:29; Ebr 3:17; Yud 5
[r]**10:6** 1Kor 9:11; Hes 11:4, 34
[s]**10:7** Kut 32:4-19; 1Kor 9:14; Kut 32:6
[t]**10:8** Hes 25:1-9

tusifanye uzinzi kama baadhi yao
walivyofanya, wakafa watu 23,000 kwa
siku moja. [9] [a]Wala tusimjaribu Kristo, kama
baadhi yao walivyofanya, wakafa kwa
kuumwa na nyoka. [10] [b]Msinung'unike kama
baadhi yao walivyofanya, wakaangamizwa
na mharabu.
[11] [c]Mambo haya yote yaliwapata wao
ili yawe mifano kwa wengine, nayo
yaliandikwa ili yatuonye sisi ambao
mwisho wa nyakati umetufikia. [12] [d]Hivyo,
yeye ajidhaniaye amesimama, aangalie
asianguke. [13] [e]Hakuna jaribu lolote
lililowapata ambalo si la kawaida kwa
wanadamu. Naye Mungu ni mwaminifu;
hataruhusu mjaribiwe kupita mnavyoweza.
Lakini mnapojaribiwa atawapa njia ya
kutokea ili mweze kustahimili.

*Karamu Za Sanamu Na Meza Ya Bwana*

[14] [f]Kwa hiyo wapenzi wangu, zikimbieni
ibada za sanamu. [15] Nasema watu wenye
ufahamu, amueni wenyewe kuhusu haya
niyasemayo. [16] [g]Je, kikombe cha baraka
ambacho tunakibariki, si ushirika katika
damu ya Kristo? Mkate tuumegao, si
ushirika wa mwili wa Kristo? [17] [h]Kwa kuwa
mkate ni mmoja, sisi tulio wengi tu mwili
mmoja, kwa kuwa wote twashiriki mkate
mmoja.
[18] [i]Waangalieni watu wa Israeli: Je, wale
wote walao dhabihu si ni wale watendao
kazi madhabahuni? [19] [j]Je, nina maana
kwamba kafara iliyotolewa kwa sanamu
ni kitu chenye maana yoyote? Au kwamba
sanamu ni kitu chenye maana yoyote? [20] [k]La
hasha! Lakini kafara za watu wasiomjua
Mungu hutolewa kwa mashetani, wala
si kwa Mungu. Nami sitaki ninyi mwe
na ushirika na mashetani. [21] [l]Hamwezi
kunywa katika kikombe cha Bwana na cha
mashetani pia. Hamwezi kuwa na sehemu
katika meza ya Bwana na katika meza ya
mashetani pia. [22] [m]Je, tunataka kuamsha
wivu wa Bwana? Je, sisi tuna nguvu kuliko
yeye?

*Fanyeni Yote Kwa Utukufu Wa Mungu*

[23] [n]"Vitu vyote ni halali," lakini si vitu
vyote vilivyo na faida. "Vitu vyote ni halali,"
lakini si vyote vinavyojenga. [24] [o]Mtu yeyote
asitafute yaliyo yake mwenyewe, bali kila
mtu atafute yale yanayowafaa wengine.
[25] [p]Kuleni chochote kinachouzwa sokoni,
bila kuuliza swali lolote kwa ajili ya
dhamiri. [26] [q]Kwa maana, "Dunia na vyote
vilivyomo ni mali ya Bwana."
[27] [r]Kama ukikaribishwa chakula na mtu
asiyeamini nawe ukikubali kwenda, kula
kila kitu kitakachowekwa mbele yako
bila kuuliza maswali kwa ajili ya dhamiri.
[28] [s]Lakini kama mtu yeyote akikuambia,
"Hiki kimetolewa kafara kwa sanamu," basi
usikile kwa ajili ya huyo aliyekuambia na
kwa ajili ya dhamiri. [29] Nina maana dhamiri
ya huyo aliyekuambia, wala si kwa ajili
ya dhamiri yako. Lakini kwa nini uhuru
wangu uhukumiwe na dhamiri ya mtu
mwingine? [30] [t]Kama nikila kwa shukrani,
kwa nini nashutumiwa kwa kile ambacho
kwa hicho ninamshukuru Mungu?
[31] [u]Basi, lolote mfanyalo, kama ni kula
au kunywa, fanyeni yote kwa utukufu

[a]**10:9** Kut 17:2; Za 78:18; 95:9; 106:14; Hes 21:5-6
[b]**10:10** Hes 16:41; 17:5, 10; 16:49; Kut 12:23; 1Nya 21:15; Ebr 11:28
[c]**10:11** Rum 4:24; 13:11; 1Kor 10:6; 1Pet 4:7
[d]**10:12** Rum 11:20; 2Kor 1:24
[e]**10:13** 1Kor 1:9; 2Pet 2:9
[f]**10:14** Ebr 6:9; 1Pet 2:11; 1Yn 2:9; 5:21; Yud 3
[g]**10:16** Mt 14:19; 26:26-28; 1Kor 11:25
[h]**10:17** Rum 12:5; 1Kor 12:27
[i]**10:18** Law 7:6, 14, 15
[j]**10:19** 1Kor 8:4; Rum 12:5; 1Kor 12:27
[k]**10:20** Kum 32:17; Law 17:7; Za 107:37; Ufu 9:20
[l]**10:21** 2Kor 6:15-16; Kum 32:38; Mal 1:7, 12
[m]**10:22** Kum 32:16, 21; 1Fal 14:22; Za 78:58; Yer 44:8; Mhu 6:10; Isa 45:9
[n]**10:23** 1Kor 6:12
[o]**10:24** Rum 15:1-2; 1Kor 13:5; Flp 2:4, 21
[p]**10:25** Mdo 10:15; 1Kor 8:7
[q]**10:26** Za 24:1; Kut 9:29; 19:5; Ay 41:11; Za 50:12; 1Tim 4:4
[r]**10:27** Lk 10:7
[s]**10:28** 1Kor 8:7, 10-12; Kum 10:14
[t]**10:30** Rum 14:6; 1Tim 4:3, 4
[u]**10:31** Zek 14:21; Kol 3:17; 1Pet 4:11

wa Mungu. 32 [a]Msiwe kikwazo kwa mtu
yeyote, wawe Wayahudi au Wayunani, au
kwa kanisa la Mungu, 33 [b]kama hata mimi
ninavyojaribu kumpendeza kila mtu kwa
kila namna. Kwa maana sitafuti mema
kwa ajili yangu mwenyewe bali kwa ajili
ya wengi, ili waweze kuokolewa.

11 [c]Igeni mfano wangu, kama ninavyouiga
mfano wa Kristo.

*Utaratibu Katika Kuabudu*

2 [d]Ninawasifu kwa kuwa mnanikumbuka
katika kila jambo na kwa kushika
mafundisho niliyowapa.

3 [e]Napenda mfahamu kwamba kichwa cha
kila mwanaume ni Kristo, na kichwa cha
mwanamke ni mwanaume, nacho kichwa
cha Kristo ni Mungu. 4 [f]Kila mwanaume
anayeomba au kutoa unabii akiwa amefunika
kichwa chake, anakiaibisha kichwa chake.
5 [g]Naye kila mwanamke anayeomba au
kutoa unabii pasipo kufunika kichwa
chake, anakiaibisha kichwa chake, kwani
ni sawa na yeye aliyenyoa nywele. 6 [h]Kama
mwanamke hatajifunika kichwa chake, basi
inampasa kunyoa nywele zake. Lakini kama
ni aibu kwa mwanamke kukata au kunyoa
nywele zake, basi afunike kichwa chake.
7 [i]Haimpasi mwanaume kufunika kichwa
chake kwa kuwa yeye ni mfano wa Mungu
na utukufu wa Mungu, lakini mwanamke
ni utukufu wa mwanaume. 8 [j]Kwa maana
mwanaume hakutoka kwa mwanamke,
bali mwanamke alitoka kwa mwanaume.
9 [k]Wala mwanaume hakuumbwa kwa ajili
ya mwanamke, bali mwanamke kwa ajili
ya mwanaume. 10 [l]Kwa sababu hii na kwa
sababu ya malaika, inampasa mwanamke
awe na ishara ya mamlaka juu yake.

11 Lakini katika Bwana, mwanamke
hajitegemei pasipo mwanaume na
mwanaume hajitegemei pasipo mwanamke.
12 [m]Kama vile mwanamke alivyoumbwa
kutoka kwa mwanaume, vivyo hivyo
mwanaume huzaliwa na mwanamke.
Lakini vitu vyote vyatoka kwa Mungu.
13 Hukumuni ninyi wenyewe: Je, inafaa
kwa mwanamke kumwomba Mungu bila
kufunika kichwa chake? 14 Je, maumbile
ya asili hayatufundishi kuwa ni aibu
kwa mwanaume kuwa na nywele ndefu?
15 Lakini mwanamke akiwa na nywele ndefu
ni utukufu kwake? Kwa maana mwanamke
amepewa nywele ndefu ili kumfunika.
16 [n]Kama mtu anataka kubishana juu ya
jambo hili, sisi wala makanisa ya Mungu
hatutambui desturi nyingine.

*Matumizi Mabaya Ya Meza Ya Bwana*

17 [o]Basi katika maagizo yafuatayo, siwezi
kuwasifu, kwa sababu mkutanikapo si kwa
ajili ya faida bali kwa hasara. 18 [p]Kwanza,
mnapokutana kama kanisa, nasikia kwamba
kuna mgawanyiko miongoni mwenu, nami
kwa kiasi fulani nasadiki kuwa ndivyo
ilivyo. 19 [q]Bila shaka lazima pawe na tofauti
miongoni mwenu ili kuonyesha ni nani
anayekubaliwa na Mungu. 20 Mkutanikapo
pamoja si chakula cha Bwana mnachokula,
21 [r]kwa kuwa mnapokula, kila mmoja wenu
anakula bila kuwangoja wengine. Mmoja
hukaa njaa na mwingine analewa. 22 [s]Je,
hamna nyumbani kwenu ambako mnaweza
kula na kunywa? Au mnalidharau kanisa
la Mungu na kuwadhalilisha wale wasio na
kitu? Niwaambie nini? Je, niwasifu juu ya
jambo hili? La, hasha!

---

[a]**10:32** Mt 5:29; Mdo 24:16; 2Kor 6:3; 1Kor 11:16-22; 15:9; 1Tim 3:5
[b]**10:33** Rum 15:2; 1Kor 9:22; Rum 11:14
[c]**11:1** 1Kor 4:16; Rum 15:13; 1Pet 2:12
[d]**11:2** 1Kor 4:17; 15:2-3; 2The 2:15; 3:6
[e]**11:3** Efe 1:22; 5:23; Mwa 3:16
[f]**11:4** Mdo 11:27; 1Kor 12:10, 28; 14:1
[g]**11:5** Mdo 21:9; Kum 21:12
[h]**11:6** Hes 5:18; Kum 22:5
[i]**11:7** Mwa 1:29; 9:6; Yak 3:9
[j]**11:8** Mwa 2:21-23; 1Tim 2:13
[k]**11:9** Mwa 2:18
[l]**11:10** Mwa 24:65; Mhu 5:6
[m]**11:12** Rum 11:36
[n]**11:16** 1Kor 7:17; 10:32
[o]**11:17** 1Kor 11:2, 22
[p]**11:18** 1Kor 1:10-12; 3:3
[q]**11:19** 1Yn 2:19
[r]**11:21** 2Pet 2:13; Yud 23
[s]**11:22** Yak 2:6

*Kuanzishwa Kwa Meza Ya Bwana*

**(Mathayo 26:26-29; Marko 14:22-25; Luka 22:14-20)**

23 [a]Kwa maana mimi nilipokea kutoka
kwa Bwana yale niliyowapa ninyi, kwamba
Bwana Yesu, usiku ule aliposalitiwa,
alitwaa mkate, 24 [b]naye akiisha kushukuru,
akaumega, akasema, "Huu ndio mwili
wangu, uliotolewa kwa ajili yenu. Fanyeni
hivi kwa ukumbusho wangu." 25 [c]Vivyo
hivyo baada ya kula, akakitwaa kikombe,
akisema, "Kikombe hiki ni agano jipya
katika damu yangu. Fanyeni hivi kila
mnywapo, kwa ukumbusho wangu."
26 [d]Maana kila mlapo mkate huu na kunywea
kikombe hiki, mnatangaza mauti ya Bwana
mpaka ajapo.

*Kushiriki Meza Ya Bwana Isivyostahili*

27 [e]Kwa hiyo, mtu yeyote alaye mkate
huo au kukinywea kikombe hicho cha
Bwana isivyostahili, atakuwa na hatia ya
dhambi juu ya mwili na damu ya Bwana.
28 [f]Inampasa mtu ajichunguze mwenyewe,
kabla ya kula mkate na kukinywea
kikombe. 29 Kwa maana mtu yeyote alaye
na kunywa pasipo kuutambua mwili wa
Bwana, hula na kunywa hukumu juu
yake mwenyewe. 30 [g]Hii ndiyo sababu
wengi miongoni mwenu ni wagonjwa na
dhaifu na wengine wenu hata wamekufa.
31 [h]Lakini kama tungejichunguza wenyewe
tusingehukumiwa. 32 [i]Tunapohukumiwa
na Bwana, tunaadibishwa ili tusije
tukahukumiwa pamoja na ulimwengu.

33 Kwa hiyo, ndugu zangu, mkutanikapo
pamoja ili kula, mngojane. 34 [j]Kama mtu
akiwa na njaa, ale nyumbani kwake ili
mkutanapo pamoja msije mkahukumiwa.

Nami nitakapokuja nitawapa maelekezo
zaidi.

*Karama Za Rohoni*

12 [k]Basi ndugu zangu, kuhusu karama
za rohoni, sitaki mkose kufahamu.
2 [l]Mnajua kwamba mlipokuwa watu
wasiomjua Mungu, kwa njia moja au
ingine mlishawishika na kupotoshwa
mkielekezwa kwa sanamu zisizonena.
3 [m]Kwa hiyo nawaambieni ya kuwa hakuna
mtu anayeongozwa na Roho wa Mungu
anayeweza kusema, "Yesu na alaaniwe."
Pia hakuna mtu awezaye kusema, "Yesu ni
Bwana," isipokuwa ameongozwa na Roho
Mtakatifu.

4 [n]Kuna aina mbalimbali za karama,
lakini Roho ni yule yule. 5 [o]Kuna huduma
za aina mbalimbali, lakini Bwana ni yule
yule. 6 [p]Kisha kuna tofauti za kutenda kazi,
lakini ni Mungu yule yule atendaye kazi
zote kwa watu wote.

7 [q]Basi kila mmoja hupewa ufunuo wa
Roho kwa faida ya wote. 8 [r]Maana mtu
mmoja kwa Roho hupewa neno la hekima
na mwingine neno la maarifa kwa Roho
huyo huyo. 9 [s]Mtu mwingine imani kwa
huyo Roho na mwingine karama za kuponya
kwa huyo Roho mmoja. 10 [t]Kwa mwingine
matendo ya miujiza, kwa mwingine unabii
kwa mwingine kupambanua roho, kwa
mwingine aina mbalimbali za lugha, na kwa
mwingine bado, tafsiri za lugha. 11 [u]Haya
yote hufanywa na huyo huyo Roho mmoja,
Roho naye humgawia kila mtu, kama
apendavyo.

[a]**11:23** Gal 1:12; 1Kor 15:3
[b]**11:24** 1Kor 10:16
[c]**11:25** Lk 22:20; 1Kor 10:16
[d]**11:26** 1Kor 1:17; 1:7; Mt 26:29
[e]**11:27** Ebr 10:29
[f]**11:28** 2Kor 13:5; Mt 26:22
[g]**11:30** Mt 9:24; 1Kor 15:20; Efe 5:14; 1The 5:6
[h]**11:31** Za 32:5; 1Yn 1:9
[i]**11:32** Za 94:12; 118:18; Mit 3:11-12; Ebr 12:7-10; Ufu 3:19
[j]**11:34** 1Kor 4:19; Tit 1:5; 1Kor 7:17; 11:22
[k]**12:1** Rum 1:11; 1Kor 1:7; 14:1, 37; Rum 11:25
[l]**12:2** Efe 2:2; Za 115:5; Yer 10:5; Hab 2:18-19
[m]**12:3** Rum 9:3; 1Kor 16:22; Yn 13:13; 4:2-3
[n]**12:4** Rum 12:4-8; Efe 4:11; Ebr 2:4
[o]**12:5** Rum 12:6; Efe 4:11
[p]**12:6** Efe 4:6; Flp 2:13; Efe 1:23
[q]**12:7** 1Kor 14:12; Efe 4:12
[r]**12:8** 1Kor 2:6; 2Kor 8:7
[s]**12:9** Mt 17:19-20; 1Kor 13:2; Mt 10:1
[t]**12:10** Gal 3:5; Efe 4:11; 1Yn 4:1; Mk 16:17
[u]**12:11** 1Kor 11:4; Rum 12:3; Efe 4:7; 1Kor 7:7

*Mwili Mmoja, Wenye Viungo Vingi*

12 [a]Kama vile mwili ulivyo mmoja nao una viungo vingi, navyo viungo vyote vya mwili ingawa ni vingi, ni mwili mmoja, vivyo hivyo na Kristo. 13 [b]Kwa maana katika Roho mmoja wote tulibatizwa katika mwili mmoja, kama ni Wayahudi au Wayunani, kama ni watumwa au watu huru, nasi sote tulinyweshwa Roho mmoja.

14 [c]Basi mwili si kiungo kimoja, bali ni viungo vingi. 15 Kama mguu ungesema, “Kwa kuwa mimi si mkono basi mimi si wa mwili,” hiyo isingefanya huo mguu usiwe sehemu ya mwili. 16 Na kama sikio lingesema, “Kwa kuwa mimi si jicho, basi mimi si wa mwili,” hiyo isingefanya hilo sikio lisiwe sehemu ya mwili. 17 Kama mwili wote ungelikuwa jicho, kusikia kungekuwa wapi? Au kama mwili wote ungelikuwa sikio, kunusa kungekuwa wapi? 18 [d]Lakini kama ilivyo, Mungu ameweka viungo katika mwili, kila kimoja kama alivyopenda. 19 Kama vyote vingekuwa kiungo kimoja, mwili ungekuwa wapi? 20 Kama ulivyo, una viungo vingi, lakini mwili ni mmoja.

21 Jicho haliwezi kuuambia mkono, “Sina haja nawe!” Wala kichwa hakiwezi kuiambia miguu, “Sina haja na ninyi!” 22 Lakini badala yake, vile viungo vya mwili vinavyoonekana kuwa dhaifu, ndivyo ambavyo ni vya muhimu sana. 23 Navyo vile viungo tunavyoviona havina heshima, ndivyo tunavipa heshima maalum. Vile viungo vya mwili ambavyo havina uzuri, tunavipa heshima ya pekee; 24 wakati vile viungo vyenye uzuri havihitaji utunzaji wa pekee. Lakini Mungu ameviweka pamoja viungo vya mwili na akavipa heshima zaidi vile vilivyopungukiwa, 25 ili pasiwe na mafarakano katika mwili, bali viungo vyote vihudumiane kwa usawa kila kimoja na mwenzake. 26 Kama kiungo kimoja kikiumia, viungo vyote huumia pamoja nacho, kama kiungo kimoja kikipewa heshima, viungo vyote hufurahi pamoja nacho.

27 [e]Sasa ninyi ni mwili wa Kristo na kila mmoja wenu ni sehemu ya huo mwili. 28 [f]Mungu ameweka katika kanisa, kwanza mitume, pili manabii, tatu walimu, kisha watenda miujiza, pia karama za kuponya, karama za kusaidiana, karama za uongozi, aina mbalimbali za lugha. 29 Je, wote ni mitume? Je, wote ni manabii? Je, wote ni walimu? Je, wote wanatenda miujiza? 30 [g]Je, wote wana karama ya kuponya? Je, wote hunena kwa lugha mpya? Je, wote wanatafsiri? 31 [h]Basi tamanini sana karama zilizo kuu.

Nami nitawaonyesha njia iliyo bora zaidi.

*Karama Ya Upendo*

13 [i]Hata kama nitasema kwa lugha za wanadamu na za malaika, kama sina upendo, nimekuwa kengele inayolialia au toazi livumalo. 2 [j]Ningekuwa na karama ya unabii na kujua siri zote na maarifa yote, hata kama nina imani kiasi cha kuweza kuhamisha milima, kama sina upendo, mimi si kitu. 3 [k]Kama nikitoa mali yote niliyo nayo na kama nikijitolea mwili wangu uchomwe moto, kama sina upendo, hainifaidi kitu.

4 [l]Upendo huvumilia, upendo hufadhili, upendo hauoni wivu, hauna majivuno, hauna kiburi. 5 [m]Haukosi kuwa na adabu, hautafuti mambo yake, haukasiriki upesi, hauweki kumbukumbu ya mabaya. 6 [n]Upendo haufurahii mabaya bali hufurahi pamoja na kweli. 7 [o]Upendo huvumilia yote,

[a]**12:12** Rum 12:5; 1Kor 11:27
[b]**12:13** Efe 2:18; Gal 3:28; Kol 3:11; Yn 7:37-38
[c]**12:14** 1Kor 12:12, 20
[d]**12:18** 1Kor 12:28; 12:11
[e]**12:27** Efe 1:23; 4:12; Kol 1:18, 24; Rum 12:5
[f]**12:28** 1Kor 10:32; Efe 4:11; Mk 16:17; Rum 12:6-8
[g]**12:30** 1Kor 12:10
[h]**12:31** 1Kor 14:1, 39
[i]**13:1** Mk 16:17; 1Kor 13:8
[j]**13:2** Efe 4:11; Mdo 11:27; 1Kor 14:2; 2Kor 8:7; 1Kor 12:9; Mt 17:20; 21:21
[k]**13:3** Lk 19:8; Mdo 2:45; Dan 3:28
[l]**13:4** 1The 5:14; 1Kor 5:2
[m]**13:5** 1Kor 10:24; Mt 5:22; Ay 14:16-17; Mit 10:12; 7:19; 1Pet 4:8
[n]**13:6** 2The 2:12; 2Yn 4; 1:3-4
[o]**13:7** 1Kor 13:8, 13; Mit 10:12; 1Kor 9:12; Rum 15:1

huamini yote, hutumaini yote, hustahimili
yote.
8 [a]Upendo haushindwi kamwe. Lakini
ukiwepo unabii, utakoma; zikiwepo
lugha, zitakoma; yakiwepo maarifa,
yatapita. 9 [b]Kwa maana tunafahamu kwa
sehemu na tunatoa unabii kwa sehemu.
10 [c]Lakini ukamilifu ukija, yale yasiyo
kamili hutoweka. 11 [d]Nilipokuwa mtoto,
nilisema kama mtoto, niliwaza kama
mtoto, nilifikiri kama mtoto. Nilipokuwa
mtu mzima niliacha mambo ya kitoto.
12 [e]Kwa maana sasa tunaona taswira kama
kwa kioo, lakini wakati huo tutaona wazi.
Sasa nafahamu kwa sehemu, wakati huo
nitafahamu kikamilifu, kama vile mimi
ninavyofahamika kikamilifu.
13 [f]Basi sasa, yanadumu mambo haya
matatu: Imani, tumaini na upendo. Lakini
lililo kuu miongoni mwa haya matatu ni
upendo.

*Karama Za Unabii Na Lugha*

14 [g]Fuateni upendo na kutaka sana karama
za roho, hasa karama ya unabii. 2 [h]Kwa
maana mtu yeyote anayesema kwa lugha,
hasemi na wanadamu bali anasema na
Mungu. Kwa kuwa hakuna mtu yeyote
anayemwelewa, kwani anasema mambo
ya siri kwa roho. 3 [i]Lakini anayetoa unabii
anasema na watu akiwajenga, kuwatia
moyo na kuwafariji. 4 [j]Anenaye kwa lugha
hujijenga mwenyewe, bali atoaye unabii
hulijenga kanisa. 5 [k]Ningependa kila mmoja
wenu anene kwa lugha lakini ningependa
zaidi nyote mtoe unabii. Kwa kuwa yeye
atoaye unabii ni mkuu kuliko anenaye kwa
lugha, isipokuwa atafsiri, ili kanisa lipate
kujengwa.
6 [l]Sasa ndugu zangu, kama nikija kwenu
nikasema kwa lugha mpya nitawafaidia
nini kama sikuwaletea ufunuo au neno la
maarifa au unabii au mafundisho? 7 Hata
vitu visivyo na uhai vitoapo sauti, kama vile
filimbi au kinubi, mtu atajuaje ni wimbo
gani unaoimbwa kusipokuwa na tofauti
ya upigaji? 8 [m]Tena kama tarumbeta haitoi
sauti inayoeleweka, ni nani atakayejiandaa
kwa ajili ya vita? 9 Vivyo hivyo na ninyi,
kama mkinena maneno yasiyoeleweka
katika akili, mtu atajuaje mnalosema?
Kwa maana mtakuwa mnasema hewani tu.
10 Bila shaka ziko sauti nyingi ulimwenguni,
wala hakuna isiyo na maana. 11 [n]Basi kama
sielewi maana ya hiyo sauti, nitakuwa
mgeni kwa yule msemaji, naye atakuwa
mgeni kwangu. 12 [o]Vivyo hivyo na ninyi.
Kwa kuwa mnatamani kuwa na karama za
rohoni, jitahidini kuzidi sana katika karama
kwa ajili ya kulijenga kanisa.
13 [p]Kwa sababu hii, yeye anenaye kwa
lugha na aombe kwamba apate kutafsiri
kile anachonena. 14 [q]Kwa maana nikiomba
kwa lugha, roho yangu inaomba, lakini akili
yangu haina matunda. 15 [r]Nifanyeje basi?
Nitaomba kwa roho, na pia nitaomba kwa
akili yangu. Nitaimba kwa roho na nitaimba
kwa akili yangu pia. 16 [s]Ikiwa unabariki
kwa roho, mtu mwingine atakayejikuta
miongoni mwa hao wasiojua, atawezaje
kusema "Amen" katika kushukuru kwako,
wakati haelewi unachosema? 17 [t]Mnaweza
kuwa mnatoa shukrani kweli, sawa, lakini
huyo mtu mwingine hajengeki.
18 Namshukuru Mungu kwamba mimi
nanena kwa lugha kuliko ninyi nyote.

[a]**13:8** 1Kor 13:2; 1Pet 4:8
[b]**13:9** 1Kor 8:2
[c]**13:10** Flp 3:12
[d]**13:11** Za 131:2
[e]**13:12** Ay 26:14; 36:26; Mwa 32:30; Ay 19:26; 1Yn 3:2; 1Kor 8:2; 8:3; Gal 4:9
[f]**13:13** Rum 5:2-5; Gal 5:5-6; Efe 4:25; Kol 1:4-5; 1The 1:3; Ebr 6:10-12; Mt 22:37-40; 1Kor 16:14; Gal 5:6; 1Yn 4:7-12, 16
[g]**14:1** 1Kor 16:14; 12:31; Efe 4:11
[h]**14:2** Mk 16:17; 1Kor 13:2
[i]**14:3** Rum 14:19; 1Kor 14:31; 14:4, 5, 12
[j]**14:4** Mk 16:17; 1Kor 13:2
[k]**14:5** Hes 11:29; 1Kor 1:3
[l]**14:6** Efe 1:17; 2Kor 8:7; Rum 6:17
[m]**14:8** Hes 10:9; Yer 4:19
[n]**14:11** Mwa 11:7
[o]**14:12** 1Kor 12:1
[p]**14:13** 1Kor 14:2
[q]**14:14** 1Kor 14:2
[r]**14:15** Efe 5:19; Kol 3:16
[s]**14:16** Kum 27:15-26; 1Nya 16:36; Neh 8:6; Za 106:48; Ufu 5:14; 7:12; Mt 14:19; 1Kor 11:24
[t]**14:17** 1Kor 14:3

19 [a]Lakini ndani ya kanisa ni afadhali
niseme maneno matano ya kueleweka
ili niwafundishe wengine kuliko kusema
maneno 10,000 kwa lugha.
20 [b]Ndugu zangu, msiwe kama watoto
katika kufikiri kwenu, afadhali kuhusu
uovu mwe kama watoto wachanga, lakini
katika kufikiri kwenu, mwe watu wazima.
21 [c]Katika Sheria imeandikwa kwamba:

“Kupitia kwa watu wenye lugha
ng’eni
na kupitia midomo ya wageni,
nitasema na watu hawa,
lakini hata hivyo
hawatanisikiliza,”
asema Bwana.

22 [d]Basi kunena kwa lugha ni ishara, si
kwa watu waaminio, bali kwa wasioamini,
wakati unabii si kwa ajili ya wasioamini,
bali kwa ajili ya waaminio. 23 [e]Kwa hiyo
kama kanisa lote likikutana na kila mmoja
akanena kwa lugha, kisha wakaingia wageni
wasioelewa wasioamini, je, hawatasema
kwamba wote mna wazimu? 24 [f]Lakini
kama mtu asiyeamini au asiyeelewa
akiingia wakati kila mtu anatoa unabii,
ataaminishwa na watu wote kuwa yeye ni
mwenye dhambi na kuhukumiwa na wote,
25 [g]nazo siri za moyo wake zitawekwa wazi.
Kwa hiyo ataanguka chini na kumwabudu
Mungu akikiri, “Kweli Mungu yuko katikati
yenu!”

### *Kumwabudu Mungu Kwa Utaratibu*

26 [h]Basi tuseme nini ndugu zangu?
Mnapokutana pamoja, kila mmoja ana
wimbo, au neno la mafundisho, au ufunuo,
lugha mpya au atatafsiri. Mambo yote
yatendeke kwa ajili ya kulijenga kanisa.
27 Kama mtu yeyote akinena kwa lugha,
basi waseme watu wawili au watatu si
zaidi, mmoja baada ya mwingine na
lazima awepo mtu wa kutafsiri. 28 Lakini
kama hakuna mtu wa kutafsiri, hao watu
na wanyamaze kimya kanisani na wanene
na nafsi zao wenyewe na Mungu.
29 [i]Manabii wawili au watatu wanene na
wengine wapime yale yasemwayo. 30 [j]Kama
mtu yeyote aliyeketi karibu, akipata ufunuo,
basi yule wa kwanza na anyamaze. 31 Kwa
maana wote mnaweza kutoa unabii, mmoja
baada ya mwingine, ili kila mtu apate
kufundishwa na kutiwa moyo. 32 [k]Roho za
manabii huwatii manabii. 33 [l]Kwa maana
Mungu si Mungu wa machafuko bali ni
Mungu wa amani.
Kama ilivyo katika makusanyiko yote ya
watakatifu, 34 [m]wanawake wanapaswa kuwa
kimya kanisani. Hawaruhusiwi kusema,
bali wanyenyekee kama sheria isemavyo.
35 [n]Kama wakitaka kuuliza kuhusu jambo
lolote, wawaulize waume zao nyumbani.
Kwa maana ni aibu kwa mwanamke
kuzungumza kanisani.
36 [o]Je, neno la Mungu lilianzia kwenu?
Au ni ninyi tu ambao neno la Mungu
limewafikia? 37 [p]Kama mtu yeyote akidhani
kwamba yeye ni nabii, au ana karama za
rohoni, basi na akubali kwamba haya
ninayoandika ni maagizo kutoka kwa
Bwana. 38 Kama mtu akipuuza jambo hili
yeye mwenyewe atapuuzwa.
39 [q]Kwa hiyo ndugu zangu, takeni sana
kutoa unabii na msikataze watu kusema
kwa lugha. 40 [r]Lakini kila kitu kitendeke
kwa heshima na kwa utaratibu.

---

[a]**14:19** 1Kor 14:6
[b]**14:20** 1Kor 3:11; Efe 4:14; Ebr 5:12-13; 1Pet 2:2; Yer 4:22; Mt 10:16; Rum 16:19
[c]**14:21** Yn 10:34; Kum 28:49; Isa 28:11-12
[d]**14:22** 1Kor 14:1
[e]**14:23** Mdo 2:13
[f]**14:24** Mdo 4:13
[g]**14:25** Rum 2:16; Zek 8:23; Isa 45:14
[h]**14:26** Kum 7:1; 1Kor 12:7-10; Efe 5:19; Rum 14:19
[i]**14:29** 1Kor 13:2; 12:10
[j]**14:30** 1The 5:19, 20
[k]**14:32** 1Yn 4:1
[l]**14:33** Rum 15:33; 1Kor 7:17; 10:32; Mdo 9:13
[m]**14:34** 1Kor 11:5, 13; Efe 5:22; 1Tim 2:11-12
[n]**14:35** 1Tim 2:11-12; Mwa 3:16
[o]**14:36** Ebr 4:12
[p]**14:37** Mdo 11:27; 1Kor 13:2; 2Kor 10:7; 1Kor 2:15; 1Yn 4:6
[q]**14:39** 1Kor 12:31; Efe 4:11
[r]**14:40** Kol 2:5

*Kufufuka Kwa Kristo*

15 [a]Basi ndugu zangu nataka niwakumbushe kuhusu Injili niliyowahubiria, mkaipokea na ambayo katika hiyo mmesimama. 2 [b]Kwa Injili hii mnaokolewa mkishikilia kwa uthabiti neno nililowahubiria ninyi. La sivyo, mmeamini katika ubatili.

3 [c]Kwa maana yale niliyopokea ndiyo niliyowapa ninyi, kama yenye umuhimu wa kwanza: Kwamba Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yasemavyo Maandiko,
4 [d]ya kuwa alizikwa na alifufuliwa siku ya tatu, kama yasemavyo Maandiko, 5 [e]na kwamba alimtokea Kefa,[f] kisha akawatokea wale kumi na wawili. 6 [g]Baadaye akawatokea wale ndugu waumini zaidi ya 500 kwa pamoja, ambao wengi wao bado wako hai, ingawa wengine wamelala. 7 [h]Ndipo akamtokea Yakobo na kisha mitume wote.
8 [i]Mwisho wa wote, akanitokea mimi pia, ambaye ni kama aliyezaliwa si kwa wakati wake.

9 [j]Kwa maana mimi ndiye mdogo kuliko mitume wote, nisiyestahili kuitwa mtume, kwa sababu nililitesa kanisa la Mungu. 10 [k]Lakini kwa neema ya Mungu nimekuwa hivi nilivyo na neema yake kwangu haikuwa kitu bure. Bali nilizidi sana kufanya kazi kuliko mitume wote, lakini haikuwa mimi, bali ni ile neema ya Mungu iliyokuwa pamoja nami. 11 [l]Hivyo basi, kama ilikuwa mimi au wao, hili ndilo tunalohubiri, na hili ndilo mliloamini.

*Ufufuo Wa Wafu*

12 [m]Basi kama tumehubiri ya kwamba Kristo alifufuliwa kutoka kwa wafu, mbona baadhi yenu mnasema hakuna ufufuo wa wafu? 13 Lakini kama hakuna ufufuo wa wafu, basi hata Kristo hakufufuliwa. 14 [n]Tena ikiwa Kristo hakufufuliwa kutoka kwa wafu, kuhubiri kwetu kumekuwa ni bure na imani yenu ni batili. 15 [o]Zaidi ya hayo, twaonekana kuwa mashahidi wa uongo kuhusu Mungu, kwa sababu tumeshuhudia kumhusu Mungu kwamba alimfufua Kristo kutoka kwa wafu, lakini hilo haliwezi kuwa kweli kama wafu hawafufuliwi. 16 [p]Kwa kuwa kama wafu hawafufuliwi, basi hata Kristo hajafufuka.
17 [q]Tena kama Kristo hajafufuliwa, imani yenu ni batili; nanyi bado mko katika dhambi zenu. 18 [r]Hivyo basi, wote waliolala katika Kristo wamepotea. 19 [s]Ikiwa tumaini letu ndani ya Kristo ni kwa ajili ya maisha haya tu, sisi tunastahili kuhurumiwa kuliko watu wote.

20 [t]Lakini kweli Kristo amefufuliwa kutoka kwa wafu, tunda la kwanza la wale wote waliolala. 21 [u]Kwa maana kama vile mauti ilivyokuja kwa njia ya mtu mmoja, vivyo hivyo, ufufuo wa wafu umekuja kwa njia ya mtu mmoja. 22 [v]Kwa maana kama vile katika Adamu watu wote wanakufa, vivyo hivyo katika Kristo wote watafanywa hai. 23 [w]Lakini kila mmoja kwa wakati wake: Kristo, tunda la kwanza kisha, wale walio wake, wakati atakapokuja. 24 [x]Ndipo mwisho utafika, wakati atakapomkabidhi Mungu Baba ufalme, akiisha angamiza kila utawala na kila mamlaka na nguvu.
25 [y]Kwa maana lazima Kristo atawale mpaka awe amewaweka adui zake wote

---

[a]**15:1** Isa 40:9; Rum 2:16; 1Kor 3:6
[b]**15:2** Rum 1:16; 11:22
[c]**15:3** Gal 1:12; 1Kor 11:2; Isa 53:5; Yn 1:29; Gal 1:4; 1Pet 2:24; Mt 26:24; Lk 24:27; Mdo 17:2; 26:22; 23
[d]**15:4** Mt 27:59-61; Mdo 2:24; Mt 16:21; Yn 2:21-22
[e]**15:5** Lk 24:34-43; Mk 16:14
[f]5 Yaani Petro.
[g]**15:6** Mt 9:24
[h]**15:7** Mdo 15:13; Lk 24:33-37; Mdo 1:3-4
[i]**15:8** Mdo 9:3-6; 1Kor 9:1; Gal 1:16
[j]**15:9** 2Kor 12:11; Efe 3:8; 1Tim 1:15; Mdo 8:3; 1Kor 10:32
[k]**15:10** Rum 3:24; 12:3; 2Kor 11:23; Kol 1:29; Flp 2:13
[l]**15:11** Gal 2:6
[m]**15:12** Yn 11:24; Mdo 17:32; 23:8; 2Tim 2:18
[n]**15:14** 1The 4:14
[o]**15:15** Mdo 2:24; 4:10, 33; 13:30
[p]**15:16** 1Kor 6:14
[q]**15:17** Rum 4:25
[r]**15:18** Mt 9:24
[s]**15:19** 1Kor 4:9
[t]**15:20** 1Pet 1:3; Mdo 26:23; Ufu 1:5; Mt 9:24
[u]**15:21** Rum 5:12
[v]**15:22** Rum 5:14-18; 1Kor 6:14
[w]**15:23** 1The 2:19; 1Kor 3:23
[x]**15:24** Dan 2:44; 7:14; 2Pet 1:11; Rum 8:38
[y]**15:25** Isa 9:7; 52:7; Mt 22:44

chini ya miguu yake. 26 [a]Adui wa mwisho
atakayeangamizwa ni mauti. 27 [b]Kwa
maana Mungu “ameweka vitu vyote chini
ya miguu yake.” Lakini isemapo kwamba
“vitu vyote” vimewekwa chini yake, ni wazi
kwamba Mungu aliyetiisha vitu vyote chini
ya Kristo hayumo miongoni mwa hivyo
vilivyotiishwa. 28 [c]Atakapokuwa amekwisha
kuyafanya haya, ndipo Mwana mwenyewe
atatiishwa chini yake yeye aliyetiisha vitu
vyote, ili Mungu awe yote katika yote.

29 Basi kama hakuna ufufuo, watafanyaje
wale wabatizwao kwa ajili ya wafu? Kama
wafu hawafufuliwi kamwe, mbona watu
wanabatizwa kwa ajili yao? 30 [d]Nasi kwa
upande wetu kwa nini tunajihatarisha
kila saa? 31 [e]Kama majivuno yangu kwa
ajili yenu katika Kristo Yesu Bwana wetu
ni kweli, ndugu zangu, ninakufa kila siku.
32 [f]Kama kwa sababu za kibinadamu tu
nilipigana na wanyama wakali huko Efeso,
ningekuwa nimepata faida gani? Kama
wafu hawafufuliwi,

“Tuleni na kunywa,
kwa kuwa kesho tutakufa.”

33 [g]Msidanganyike: “Ushirika na watu
wabaya huharibu tabia njema.” 34 [h]Zindukeni
mwe na akili kama iwapasavyo, wala
msitende dhambi tena; kwa maana watu
wengine hawamjui Mungu. Nasema mambo
haya ili mwone aibu.

*Mwili Wa Ufufuo*

35 [i]Lakini mtu anaweza kuuliza, “Wafu
wafufuliwaje? Watakuwa na mwili wa
namna gani?” 36 [j]Ninyi wapumbavu
kiasi gani? Mpandacho hakiwi hai kama
hakikufa. 37 Mpandapo, hampandi mwili
ule utakao kuwa, bali mwapanda mbegu
tu, pengine ya ngano au ya kitu kingine.
38 [k]Lakini Mungu huipa mbegu umbo kama
alivyokusudia mwenyewe na kila aina ya
mbegu huipa umbo lake. 39 Kwa maana
nyama zote si za aina moja. Binadamu
wana nyama ya aina moja, wanyama wana
aina nyingine, kadhalika ndege na samaki
wana nyama tofauti. 40 Pia kuna miili ya
mbinguni na miili ya duniani, lakini fahari
wa ile miili ya mbinguni ni wa aina moja
na fahari wa ile miili ya duniani ni wa aina
nyingine. 41 [l]Jua lina fahari ya aina moja,
mwezi nao una fahari yake na nyota pia,
nazo nyota hutofautiana katika fahari.

42 [m]Hivyo ndivyo itakavyokuwa wakati wa
ufufuo wa wafu. Ule mwili wa kuharibika
uliopandwa, utafufuliwa usioharibika,
43 [n]unapandwa katika aibu, unafufuliwa
katika utukufu, unapandwa katika udhaifu,
unafufuliwa katika nguvu, 44 [o]unapandwa
mwili wa asili, unafufuliwa mwili wa
kiroho.

Kama kuna mwili wa asili, basi kuna mwili
wa kiroho pia. 45 [p]Kwa hiyo imeandikwa,
“Mtu wa kwanza Adamu alifanyika kiumbe
hai”; Adamu wa mwisho, yeye ni roho
iletayo uzima. 46 Lakini si ule wa kiroho
uliotangulia, bali ni ule wa asili, kisha ule
wa kiroho. 47 Mtu wa kwanza aliumbwa
kwa mavumbi ya ardhini, mtu wa pili
alitoka mbinguni. 48 [q]Kama vile alivyokuwa
yule wa ardhini, ndivyo walivyo wale
walio wa ardhini; na kwa vile alivyo mtu
yule aliyetoka mbinguni, ndivyo walivyo
wale walio wa mbinguni. 49 [r]Kama vile
tulivyochukua mfano wa mtu wa ardhini,
ndivyo tutakavyochukua mfano wa yule
mtu aliyetoka mbinguni.

50 [s]Ndugu zangu nisemalo ni hili:
nyama na damu haviwezi kuurithi

[a]**15:26** 2Tim 1:10; Ufu 20:14; 21:4
[b]**15:27** Za 8:6; Mt 22:44; 28:18
[c]**15:28** Flp 3:21; 1Kor 3:23
[d]**15:30** 2Kor 11:26
[e]**15:31** Rum 8:36
[f]**15:32** 2Kor 1:8; Mdo 18:19; Isa 22:13; Lk 12:19
[g]**15:33** 1Kor 6:9; Mit 22:24-25
[h]**15:34** Gal 4:8; 1Kor 4:8; 4:14
[i]**15:35** Rum 9:19; Eze 37:3
[j]**15:36** Lk 11:40; 12:20; Yn 12:24
[k]**15:38** Mwa 1:11
[l]**15:41** Za 19:4-6; 8:1-3
[m]**15:42** Dan 12:3; Mt 13:43
[n]**15:43** Flp 3:21; Kol 3:4
[o]**15:44** 1Kor 15:50
[p]**15:45** Mwa 2:7; Rum 5:14; Yn 5:21; 6:57-58; Rum 8:2
[q]**15:48** Flp 3:20-21
[r]**15:49** Mwa 5:3; Rum 8:29
[s]**15:50** Efe 6:12; Ebr 2:14; Mt 25:34

ufalme wa Mungu, wala kuharibika
kurithi kutokuharibika. 51 [a]Sikilizeni,
nawaambia siri: Sote hatutalala, lakini
sote tutabadilishwa 52 [b]ghafula, kufumba na
kufumbua, parapanda ya mwisho itakapolia.
Kwa kuwa parapanda italia, nao wafu
watafufuliwa na miili isiyoharibika, nasi
tutabadilishwa. 53 [c]Kwa maana mwili huu
wa kuharibika lazima uvae kutokuharibika,
nao huu wa kufa lazima uvae kutokufa.
54 [d]Kwa hiyo, mwili huu wa kuharibika
utakapovaa kutokuharibika, nao huu mwili
wa kufa utakapovaa kutokufa, ndipo lile
neno lililoandikwa litakapotimia: "Mauti
imemezwa kwa kushinda."

55 [e]"Kuko wapi, ee mauti, kushinda
kwako?
Uko wapi, ee mauti, uchungu
wako?"

56 [f]Uchungu wa mauti ni dhambi na nguvu
ya dhambi ni sheria. 57 [g]Lakini ashukuriwe
Mungu, yeye atupaye ushindi kwa njia ya
Bwana wetu Yesu Kristo.
58 [h]Kwa hiyo, ndugu zangu wapenzi,
simameni imara, msitikisike, mzidi sana
katika kuitenda kazi ya Bwana, kwa maana
mnajua ya kuwa, kazi yenu katika Bwana
si bure.

### *Changizo Kwa Ajili Ya Watakatifu*

16 [i]Basi kuhusu changizo kwa ajili ya
watakatifu: Kama nilivyoyaagiza
makanisa ya Galatia, fanyeni vivyo hivyo.
2 [j]Siku ya kwanza ya kila juma, kila mmoja
wenu atenge kiasi cha fedha, kulingana na
mapato yake na fedha hizo aziweke akiba, ili
nitakapokuja pasiwe na lazima ya kufanya
mchango. 3 [k]Kwa hiyo nitakapowasili,
nitawapa wale mtakaowachagua barua za
kuwatambulisha, ili kuwatuma wapeleke
zawadi zenu huko Yerusalemu. 4 [l]Kama
ikionekana ni vyema na mimi niende, basi
hao watu watafuatana nami.

### *Mahitaji Binafsi*

5 [m]Baada ya kupitia Makedonia nitakuja
kwenu, maana ninakusudia kupitia
Makedonia. 6 [n]Huenda nitakaa nanyi kwa
muda, au hata kukaa nanyi kipindi chote
cha baridi, ili mweze kunisaidia katika safari
yangu, popote niendapo. 7 [o]Kwa maana
sitaki niwaone sasa na kupita tu; natarajia
kuwa nanyi kwa muda wa kutosha, kama
Bwana akipenda. 8 [p]Lakini nitakaa Efeso
mpaka wakati wa Pentekoste, 9 [q]kwa maana
mlango mkubwa umefunguliwa kwangu
kufanya kazi yenye matunda, nako huko
kuna adui wengi wanaonipinga.
10 [r]Ikiwa Timotheo atakuja kwenu,
hakikisheni kwamba hana hofu yoyote
akiwa nanyi, kwa sababu anafanya kazi
ya Bwana, kama mimi nifanyavyo. 11 [s]Basi
asiwepo mtu atakayekataa kumpokea.
Msafirisheni kwa amani ili aweze kunijia
tena. Namtarajia pamoja na ndugu.
12 [t]Basi kwa habari za ndugu yetu Apolo,
nimemsihi kwa bidii aje kwenu pamoja na
hao ndugu. Ingawa alikuwa hapendi kabisa
kuja sasa, lakini atakuja apatapo nafasi.

### *Maneno Ya Mwisho*

13 [u]Kesheni, simameni imara katika imani,
fanyeni kiume, kuweni mashujaa kuweni
hodari. 14 [v]Fanyeni kila kitu katika upendo.

[a]**15:51** 1Kor 13:2; 14:2; Mt 9:24; 2Kor 5:4; Flp 3:21
[b]**15:52** Mt 24:31; Yn 5:25
[c]**15:53** 2Kor 5:2-4
[d]**15:54** Isa 25:8; Ebr 2:14; Ufu 20:14
[e]**15:55** Hos 13:14; Isa 25:8
[f]**15:56** Rum 5:12; 14:15
[g]**15:57** 2Kor 2:14; Rum 8:37; Ebr 2:14-15
[h]**15:58** 1Kor 16:10; Isa 65:23
[i]**16:1** Mdo 24:17; 9:13; 16:6
[j]**16:2** Mdo 20:7; 2Kor 9:4-5
[k]**16:3** 2Kor 3:1; 8:18-19
[l]**16:4** 2Kor 8:4, 19
[m]**16:5** 1Kor 4:19; Mdo 16:9
[n]**16:6** Rum 15:24; Tit 3:13
[o]**16:7** Mdo 18:21
[p]**16:8** Mdo 18:19; 2:1
[q]**16:9** Mdo 14:27; 2Kor 2:12; Kol 4:3; Ufu 3:8; Mdo 19:9
[r]**16:10** Mdo 16:1; 19:22; Rum 16:21; Flp 2:20, 22; 1The 3:2
[s]**16:11** 1Tim 4:12; 2Kor 1:16; 3Yn 6; Mdo 19:9
[t]**16:12** Mdo 18:24; 1Kor 1:12
[u]**16:13** 1Kor 1:8; 2Kor 1:21; Gal 5:1; Flp 1:27; 1The 3:8; Tit 1:9; Efe 6:10
[v]**16:14** 1Kor 14:1

15 [a]Ninyi mnajua kwamba watu wa
nyumbani mwa Stefana ndio waliokuwa
wa kwanza kuamini katika Akaya, nao
wamejitoa kwa ajili ya kuwahudumia
watakatifu. Ndugu nawasihi, 16 [b]mjitie katika
kuwahudumia watu kama hawa na kila
mmoja aingiaye kwenye kazi na kuifanya
kwa bidii. 17 [c]Nilifurahi wakati Stefana,
Fortunato na Akaiko walipofika, kwa
sababu wamenipatia yale niliyopungukiwa
kutoka kwenu. 18 [d]Kwa kuwa waliiburudisha
roho yangu na zenu pia. Watu kama hawa
wanastahili kutambuliwa.

*Salamu Za Mwisho*

19 [e]Makanisa ya Asia yanawasalimu.
Akila na Prisila,[f] pamoja na kanisa lililoko
nyumbani kwao wanawasalimu sana katika
Bwana. 20 [g]Ndugu wote walioko hapa
wanawasalimu. Salimianeni kwa busu
takatifu.

21 [h]Mimi, Paulo, naandika salamu hizi
kwa mkono wangu mwenyewe.

22 [i]Kama mtu yeyote hampendi Bwana
Yesu Kristo, na alaaniwe. Bwana wetu,
njoo.[j]

23 [k]Neema ya Bwana Yesu iwe nanyi.

24 Upendo wangu uwe nanyi nyote katika
Kristo Yesu. Amen.

---

[a]**16:15** 1Kor 1:6; Rum 16:5; Mdo 18; 12; 24; 17; 9:13
[b]**16:16** 1The 5:12; Ebr 13:17
[c]**16:17** 2Kor 11:9; Flp 2:30
[d]**16:18** Rum 15:32; Flp 1:7; 2:29
[e]**16:19** Mdo 2:9; 18:2; Rum 16:5
[f]19 Prisila kwa Kiyunani ni Priska, hivyo tafsiri nyingine zimemuita Priska.
[g]**16:20** Rum 16:16; 2Kor 13:12; 1Pet 5:14
[h]**16:21** Gal 6:11; Kol 4:18; 2The 3:17
[i]**16:22** Efe 6:24; Rum 9:3; Ufu 22:20
[j]22 Kwa Kiaramu ni *Marana tha*.
[k]**16:23** Rum 16:20

# 2 WAKORINTHO

*Salamu*

1 [a]Barua hii ni kutoka kwangu mimi Paulo,
mtume wa Kristo Yesu kwa mapenzi ya
Mungu, na Timotheo ndugu yetu,
Kwa kanisa la Mungu lililoko Korintho,
pamoja na watakatifu wote walioko Akaya
yote:
2 [b]Neema na amani itokayo kwa Mungu
Baba yetu na kwa Bwana Yesu Kristo iwe
nanyi.

*Mungu Wa Faraja Yote*

3 [c]Ahimidiwe Mungu na Baba wa Bwana
wetu Yesu Kristo, Baba wa huruma na
Mungu wa faraja yote. 4 [d]Yeye hutufariji
katika taabu zetu, ili tuweze kuwafariji
walio katika taabu yoyote kwa faraja
ambayo sisi wenyewe tumepokea kutoka
kwa Mungu. 5 [e]Kama vile mateso ya Kristo
yanavyozidi ndani ya maisha yetu, hivyo
ndivyo faraja yetu inavyofurika kwa njia ya
Kristo. 6 [f]Kama tunataabika, ni kwa ajili ya
faraja na wokovu wenu; kama tukifarijiwa,
ni kwa ajili ya faraja yenu, iwaleteayo saburi
ya mateso yale yale yanayotupata. 7 [g]Nalo
tumaini letu kwenu ni thabiti, kwa sababu
tunajua kwamba kama vile mnavyoshiriki
mateso yetu, ndivyo pia mnavyoshiriki
katika faraja yetu.
8 [h]Ndugu wapendwa, hatutaki mkose
kujua kuhusu zile taabu tulizopata huko
Asia. Kwa maana tulilemewa na mizigo sana,
kiasi cha kushindwa kuvumilia, hata tulikata
tamaa ya kuishi. 9 [i]Kwa kweli, mioyoni
mwetu tulihisi tumekabiliwa na hukumu
ya kifo, ili tusijitegemee sisi wenyewe bali
tumtegemee Mungu afufuaye wafu. 10 [j]Yeye
aliyetuokoa kwenye hatari kubwa ya kifo
na atatuokoa tena. Kwake yeye tumeweka
tumaini letu kwamba ataendelea kutuokoa.
11 [k]Kama vile mlivyoungana kusaidiana
nasi katika maombi, hivyo wengi watatoa
shukrani kwa niaba yetu kwa ajili ya baraka
za neema tulizopata kwa majibu ya maombi
ya wengi.

*Paulo Aahirisha Ziara*

12 [l]Basi haya ndiyo majivuno yetu: Dhamiri
yetu inatushuhudia kwamba tumeenenda
katika ulimwengu na hasa katika uhusiano
wetu na ninyi, katika utakatifu na uaminifu
utokao kwa Mungu. Hatukufanya hivyo
kwa hekima ya kidunia bali kwa neema
ya Mungu. 13 Kwa maana hatuwaandikii
mambo ambayo hamwezi kusoma au
kuyaelewa. Natumaini kwamba, 14 [m]kama
vile mlivyotuelewa kwa sehemu, mtakuja
kuelewa kwa ukamilifu ili mweze kujivuna
kwa ajili yetu, kama na sisi tutakavyojivuna
kwa ajili yenu katika siku ya Bwana Yesu.
15 [n]Kwa kuwa nilikuwa na uhakika wa
mambo haya, nilitaka nije kwenu kwanza,
ili mpate faida mara mbili. 16 [o]Nilipanga
kuwatembelea nikiwa safarini kwenda
Makedonia na kurudi tena kwenu nikitoka
Makedonia, ili mnisafirishe katika safari
yangu ya kwenda Uyahudi. 17 [p]Nilipopanga
jambo hili, je, nilikuwa kigeugeu? Au
ninafanya mipango yangu kwa hali ya
mwili, ili niseme, "Ndiyo, ndiyo" na "Siyo,
siyo" wakati huo huo?
18 [q]Hakika kama Mungu alivyo

[a]**1:1** 1Kor 1:11; Efe 1:1; Kol 1:1; 2Tim 1:1; Mdo 16:1; 1Kor 10:32; Mdo 18:1; 18:12
[b]**1:2** Rum 1:7; 1Kor 1:3; Gal 1:3; Flp 1:2; Kol 1:2; Flp 3:1; 1The 1:1
[c]**1:3** Efe 1:3; 1Pet 1:3; Rum 15:5
[d]**1:4** Isa 49:13; 51:12; 66:13; 2Kor 7:6-13
[e]**1:5** Rum 8:17; 2Kor 4:10; Gal 6:17; Flp 3:10; Kol 1:24; 1Pet 4:13
[f]**1:6** 2Kor 4:15; 4:17
[g]**1:7** 2Kor 1:5; Rum 8:17; 2Tim 2:12
[h]**1:8** Rum 11:25; 1Kor 15:32; Mdo 2:9
[i]**1:9** Yer 17:5-7; Yn 5:21
[j]**1:10** Rum 15:31; 1Tim 4:10
[k]**1:11** Rum 15:30; Flp 1:19; 2Kor 4:15; 9:11
[l]**1:12** Mdo 23:11; 1The 2:10; 2Kor 2:17; 1Kor 1:17; 2:1-13
[m]**1:14** 1Kor 1:8
[n]**1:15** 1Kor 4:19; Rum 1:11-13; 15:29
[o]**1:16** 1Kor 16:5-7; Mdo 16:9; 3Yn 6; Mdo 19:2
[p]**1:17** 2Kor 10:2-3; 11:18
[q]**1:18** 1Kor 1:9

mwaminifu, maneno yetu kwenu hayajawa
“Ndiyo na Siyo.” 19 [a]Kwa kuwa Yesu Kristo,
Mwana wa Mungu, ambaye tulimhubiri
kwenu: Mimi, Silvano[b] na Timotheo,
hakuwa “Ndiyo” na “Siyo,” bali kwake
yeye siku zote ni “Ndiyo.” 20 [c]Kwa maana
ahadi zote za Mungu zilizo katika Kristo
ni “Ndiyo.” Kwa sababu hii ni kwake yeye
tunasema “Amen” kwa utukufu wa Mungu.
21 [d]Basi ni Mungu atufanyaye sisi pamoja
nanyi kusimama imara katika Kristo.
Ametutia mafuta 22 [e]kwa kututia muhuri
wake na kutupa Roho wake mioyoni mwetu
kuwa rehani kwa ajili ya kututhibitishia
kile kijacho.

23 [f]Mungu ni shahidi wangu kwamba
ilikuwa ni kwa ajili ya kuwahurumia
ninyi sikurudi Korintho. 24 [g]Si kwamba
tunatawala imani yenu, bali twatenda kazi
pamoja nanyi kwa ajili ya furaha yenu, kwa
sababu ni kwa imani mwasimama imara.

2 [h]Hivyo nilikusudia moyoni mwangu
nisifanye ziara nyingine yenye kuwaumiza
ninyi. 2 [i]Kwa kuwa kama nikiwahuzunisha
ninyi, ni nani aliyebaki wa kunifurahisha
isipokuwa ninyi ambao nimewahuzunisha?
3 [j]Niliandika hivyo kama nilivyofanya, ili
nikija nisihuzunishwe na wale watu ambao
wangenifanya nifurahi. Nina uhakika na
ninyi nyote, kwamba wote mngeshiriki
furaha yangu. 4 [k]Kwa maana niliwaandikia
kutokana na dhiki kubwa na kutaabika
sana kwa moyo wangu tena kwa machozi
mengi, shabaha yangu si ili niwasababishe
mhuzunike bali kuwaonyesha kina cha
upendo wangu kwenu.

*Msamaha Kwa Mwenye Dhambi*

5 [l]Lakini ikiwa mtu yeyote amesababisha
huzuni, kwa kiasi fulani hakunihuzunisha
mimi kama vile alivyowahuzunisha ninyi
nyote, ili nisiwe mkali kupita kiasi. 6 [m]Adhabu
hii aliyopewa na wengi inamtosha. 7 [n]Basi
sasa badala yake, inawapasa kumsamehe
na kumfariji, ili asigubikwe na huzuni
kupita kiasi. 8 Kwa hiyo, nawasihi, mpate
kuuthibitisha tena upendo wenu kwa
ajili yake. 9 [o]Sababu ya kuwaandikia ni
kuona kama mngeweza kushinda hilo
jaribio na kutii katika kila jambo. 10 [p]Kama
ninyi mkimsamehe mtu yeyote, mimi pia
nimemsamehe. Kile nilichosamehe, kama
kulikuwa na kitu chochote cha kusamehe,
nimekwisha kusamehe mbele ya Kristo kwa
ajili yenu, 11 [q]ili Shetani asitushinde. Kwa
maana hatuachi kuzijua hila zake.

*Wasiwasi Wa Paulo Huko Troa*

12 [r]Basi nilipofika Troa kuhubiri Injili ya
Kristo na kukuta kwamba Bwana alikuwa
amenifungulia mlango, 13 [s]bado nilikuwa
sina utulivu akilini mwangu kwa sababu
sikumkuta ndugu yangu Tito huko. Hivyo
niliagana nao nikaenda Makedonia.

14 [t]Lakini Mungu ashukuriwe, yeye
ambaye siku zote hutufanya tuandamane
kwa ushindi tukiwa ndani ya Kristo. Naye
kupitia kwetu hueneza kila mahali harufu
nzuri ya kumjua yeye. 15 [u]Kwa maana sisi
kwa Mungu ni harufu nzuri ya manukato ya
Kristo miongoni mwa wale wanaookolewa
na kwa wale wanaopotea. 16 [v]Kwa wale
wanaopotea, sisi ni harufu ya mauti iletayo
mauti; lakini kwa wale wanaookolewa,

[a]**1:19** Mt 4:3; Mdo 15:22; 16:1
[b]19 Yaani Sila.
[c]**1:20** Rum 15:9
[d]**1:21** 1Kor 16:13; 1Yn 2:20-27
[e]**1:22** Mwa 38:18; Hag 2:23; 2Kor 5:5
[f]**1:23** Rum 1:9; 1Kor 4:21; 2Kor 2:1-3; 13:2-10
[g]**1:24** 1Pet 5:3; Rum 11:20; 1Kor 1:5-11
[h]**2:1** 2Kor 1:23; 12:20, 21; 13:10
[i]**2:2** 2Kor 7:8
[j]**2:3** 2Kor 7:8-12; 12:21; 7:16; 8:22; Gal 5:10; 2The 3:4
[k]**2:4** 2Kor 7:8-12; 12:20, 21; 13:10
[l]**2:5** 1Kor 5:1-2; Gal 4:12; 1Kor 5:1
[m]**2:6** 1Kor 5:4-5; 2Kor 7:11
[n]**2:7** Gal 6:1; Efe 4:32; Kol 3:13
[o]**2:9** 2Kor 7:8-12; 7:15; 10:6
[p]**2:10** Lk 10:16
[q]**2:11** Mt 4:10; Lk 22:31; 2Kor 4:4; 1Pet 5:8
[r]**2:12** Rum 1:1; 2Kor 4:3-4; 8:18; 9:13; 1The 3:2; Mdo 14:21
[s]**2:13** 2Kor 7:5; 7:6-13; 8:6-23; 12:18; Gal 2:1-3; Tit 1:4; Mdo 16:9
[t]**2:14** Rum 6:17; 7:25; 1Kor 15:57; 2Kor 9:15; Eze 20:41; Efe 5:2; Flp 4:18; 2Kor 8:7
[u]**2:15** Mwa 8:21; Kut 29:18
[v]**2:16** Lk 2:34; Yn 3:36; 2Kor 3:5-6

sisi ni harufu nzuri iletayo uzima. Ni nani awezaye mambo hayo? 17 [a]Tofauti na watu wengine wengi, sisi hatufanyi biashara na Neno la Mungu kwa ajili ya kupata faida. Kinyume chake, katika Kristo tunalisema Neno la Mungu kwa unyoofu, kama watu tuliotumwa kutoka kwa Mungu.

*Wahudumu Wa Agano Jipya*

3 [b]Je, tunaanza tena kujisifu wenyewe? Au tunahitaji kupata barua za utambulisho kwenu au kutoka kwenu, kama watu wengine? 2 [c]Ninyi wenyewe ndio barua yetu iliyoandikwa katika mioyo yetu, inayojulikana na kusomwa na kila mtu.
3 [d]Nanyi mwadhihirisha wazi kwamba ninyi ni barua itokayo kwa Kristo, matokeo ya huduma yetu, ambayo haikuandikwa kwa wino bali kwa Roho wa Mungu aliye hai, si katika vibao vya mawe, bali katika vibao ambavyo ni mioyo ya wanadamu.
4 [e]Hili ndilo tumaini tulilo nalo mbele za Mungu kwa njia ya Kristo. 5 [f]Si kwamba sisi tunafikiri kuwa tunaweza kufanya jambo lolote wenyewe, lakini nguvu yetu inatoka kwa Mungu. 6 [g]Ndiye alituwezesha sisi kuwa wahudumu wa Agano Jipya: si wa andiko, bali wa Roho; kwa kuwa andiko huua bali Roho hutia uzima.

*Utukufu Wa Agano Jipya*

7 [h]Basi ikiwa ile huduma iliyoleta mauti, iliyoandikwa kwa herufi juu ya jiwe ilikuja kwa utukufu, hata Waisraeli wakawa hawawezi kuutazama uso wa Mose kwa sababu ya ule utukufu wake ingawa ulikuwa ni wa kufifia, 8 [i]je, huduma ya Roho haitakuwa na utukufu zaidi? 9 [j]Ikiwa huduma ile inayowahukumu wanadamu ina utukufu, je, ile huduma iletayo haki haitakuwa ya utukufu zaidi? 10 [k]Kwa maana kile kilichokuwa na utukufu sasa hakina utukufu ukilinganisha na huu utukufu unaozidi wa Agano Jipya. 11 Ikiwa kile kilichokuwa kinafifia kilikuja kwa utukufu, je, si zaidi utukufu wa kile kinachodumu?
12 [l]Kwa hiyo, kwa kuwa tunalo tumaini hili, tuna ujasiri sana. 13 [m]Sisi si kama Mose, ambaye ilimpasa kuweka utaji ili kufunika uso wake ili Waisraeli wasiuone ule mng'ao uliokuwa juu yake hadi ulipofifia na hatimaye kutoweka. 14 [n]Lakini akili zao zilipumbazwa, kwa maana mpaka leo utaji ule ule hufunika wakati Agano la Kale linasomwa. Huo utaji haujaondolewa, kwa maana ni katika Kristo peke yake unaondolewa. 15 [o]Hata leo Sheria ya Mose inaposomwa, utaji hufunika mioyo yao.
16 [p]Lakini wakati wowote mtu anapomgeukia Bwana, utaji unaondolewa. 17 Basi Bwana ndiye Roho. Mahali alipo Roho wa Bwana hapo pana uhuru. 18 [q]Nasi sote, tukiwa na nyuso zisizotiwa utaji tunadhihirisha utukufu wa Bwana, kama kwenye kioo. Nasi tunabadilishwa ili tufanane naye, toka utukufu hadi utukufu mkuu zaidi, utokao kwa Bwana, ambaye ndiye Roho.

*Hazina Ya Mbinguni Katika Vyombo Vya Udongo*

4 [r]Kwa hiyo, kwa kuwa tuna huduma hii kwa rehema za Mungu, hatukati tamaa. 2 [s]Tumekataa mambo ya siri na ya aibu, wala hatufuati njia za udanganyifu, tukichanganya Neno la Mungu na uongo.

[a]**2:17** Mdo 20:33; 2Kor 4:2; 1The 2:5; 1Kor 5:8; 2Kor 1:12; 12:19
[b]**3:1** Rum 16:1; 2Kor 5:12; 10:12-18; 12:11; Mdo 18:17; Rum 16:1; 1Kor 3:16
[c]**3:2** 1Kor 9:2
[d]**3:3** Mt 16:16; Kut 24:12; 31:18; 32:15-16; Mit 3:3; 7:3; Yer 31:33; Eze 36:26
[e]**3:4** Efe 3:12
[f]**3:5** 2Kor 2:16; 1Kor 15:10
[g]**3:6** Lk 22:20; Rum 2:29; 7:6; Yn 6:63
[h]**3:7** Rum 4:15; Kut 34:29-35; Isa 42:21
[i]**3:8** Gal 3; 5; 3:2
[j]**3:9** Kum 27:26; Rum 1:17; 3:21-22
[k]**3:10** Kut 34:29
[l]**3:12** Rum 5:4-5; 8:24-25; Mdo 4:29
[m]**3:13** Kut 34:33; 2Kor 3:7; Kut 34:35; Rum 10:4
[n]**3:14** Rum 11:7-8; 2Kor 4:4; Mdo 13:15; 15:21
[o]**3:15** Rum 11:23; Kut 34:35; Isa 25:7
[p]**3:16** Rum 11:23; Kut 34:34; Isa 25:7
[q]**3:18** 1Kor 13:12; Yn 17:22-24; 2Kor 4:4-6; Rum 8:29
[r]**4:1** 1Kor 7:25; 1Tim 1:13-16; Za 18:45; Isa 40:31
[s]**4:2** Rum 6:21; 1Kor 4:5; 2Kor 2:17; Ebr 4:12; 2Kor 5:11

Kinyume cha hayo, tunadhihirisha kweli
waziwazi na kujitambulisha wenyewe
kwenye dhamiri ya kila mtu mbele za
Mungu. 3 [a]Hata nayo Injili yetu kama
imetiwa utaji, ni kwa wale tu wanaopotea.
4 [b]Kwa habari yao, mungu wa dunia hii
amepofusha akili za wasioamini, ili wasione
nuru ya Injili ya utukufu wa Kristo, aliye
sura ya Mungu. 5 [c]Kwa maana hatujihubiri
sisi wenyewe ila tunamhubiri Yesu Kristo
kuwa ni Bwana na sisi ni watumishi wenu
kwa ajili ya Yesu. 6 [d]Kwa kuwa Mungu,
yeye aliyesema, “Nuru na ing’ae gizani,”
ameifanya nuru yake ing’ae mioyoni mwetu
ili kutupatia nuru ya maarifa ya utukufu wa
Mungu katika uso wa Kristo.

7 [e]Lakini tunayo hazina hii katika
vyombo vya udongo, ili ijulikane wazi
kwamba uwezo huu wa ajabu unatoka
kwa Mungu wala si kwetu. 8 [f]Twataabika
kila upande lakini hatuangamizwi; twaona
wasiwasi lakini hatukati tamaa; 9 [g]twateswa
lakini hatuachwi; twatupwa chini lakini
hatupondwi. 10 [h]Siku zote twachukua katika
mwili kufa kwake Yesu ili kwamba uzima
wa Yesu uweze kudhihirika katika miili
yetu. 11 [i]Kwa maana sisi tulio hai siku
zote tumetolewa tufe kwa ajili ya Yesu, ili
kwamba uzima wake upate kudhihirishwa
katika mwili wetu upatikanao na mauti.
12 [j]Hivyo basi, mauti inatenda kazi ndani
yetu, bali uzima unatenda kazi ndani yenu.

13 [k]Imeandikwa, “Niliamini, kwa hiyo
nimesema.” Kwa roho yule yule wa imani
pia tuliamini na hivyo tunasema, 14 [l]kwa
sababu tunajua kwamba yeye aliyemfufua
Bwana Yesu kutoka kwa wafu, atatufufua
sisi pia pamoja na Yesu na kutuleta sisi
pamoja nanyi mbele zake. 15 [m]Haya yote
ni kwa faida yenu, ili kwamba neema ile
inavyowafikia watu wengi zaidi na zaidi,
ipate kusababisha shukrani nyingi kwa
utukufu wa Mungu.

16 [n]Kwa hiyo, hatukati tamaa. Ingawa utu
wetu wa nje unachakaa, utu wetu wa ndani
unafanywa upya siku kwa siku. 17 [o]Kwa
maana dhiki yetu nyepesi iliyo ya kitambo
inatutayarisha kwa ajili ya utukufu wa
milele unaozidi kuwa mwingi kupita kiasi,
18 [p]kwa sababu hatuangalii yale yanayoweza
kuonekana bali yale yasiyoweza kuonekana.
Kwa maana yale yanayoweza kuonekana
ni ya kitambo tu, bali yale yasiyoweza
kuonekana ni ya milele.

### *Makao Yetu Ya Mbinguni*

5 [q]Kwa maana twajua kama hema yetu
ya dunia tunayoishi ikiharibiwa, tunalo
jengo kutoka kwa Mungu, nyumba iliyo
ya milele kule mbinguni, isiyojengwa kwa
mikono ya wanadamu. 2 Katika hema hii
twalia kwa uchungu, tukitamani kuvikwa
makao yetu ya mbinguni, 3 kwa kuwa
tukiisha kuvikwa hatutaonekana tena kuwa
uchi. 4 [r]Kwa kuwa tukiwa bado katika hema
hii twalia kwa uchungu na kulemewa, kwa
sababu hatutaki kuvuliwa bali kuvikwa
makao yetu ya mbinguni ili kwamba kile
kipatikanacho na mauti kimezwe na uzima.
5 [s]Basi Mungu ndiye alitufanya kwa ajili
ya jambo lilo hilo naye ametupa Roho
Mtakatifu kuwa amana, akituhakikishia
ahadi ya kile kijacho.

6 [t]Kwa hiyo siku zote tunalo tumaini, hata
ingawa tunajua kwamba wakati tukiwa
katika mwili huu, tuko mbali na Bwana,

[a]**4:3** 2Kor 2:12; 3:14; 1Kor 1:18
[b]**4:4** Yn 12:31; 1Kor 1:20; 2Kor 3:14; Yn 14:9
[c]**4:5** 1Kor 1:13; 1:23; 9:19
[d]**4:6** Mwa 1:3; Za 18:28; 2Pet 1:19
[e]**4:7** Ay 4:19; Isa 64:8; 2Tim 2:20; Amu 7:2; 1Kor 2:5; 2Kor 6:7
[f]**4:8** 2Kor 7:5; Gal 4:20
[g]**4:9** Yn 15:20; Rum 8:35; Ebr 13:5; Za 37:24; Mit 24:16
[h]**4:10** Rum 6:6; 2Kor 1:5; Rum 6:5
[i]**4:11** Rum 8:36
[j]**4:12** 2Kor 13:9
[k]**4:13** Za 116:10; 1Kor 12:29
[l]**4:14** Mdo 2:24; 1The 4:14; Efe 5:27; Kol 1:22; Yud 24
[m]**4:15** 1Kor 1:11; 9:11
[n]**4:16** Za 18:45; Rum 7:22; Za 103:5
[o]**4:17** Za 30:5; Rum 8:18; 1Pet 1:6-7
[p]**4:18** 2Kor 5:7; Rum 8:24; Ebr 11
[q]**5:1** 1Kor 15:47; Isa 38:12; 1Pet 1:13-14
[r]**5:4** 1Kor 15:33, 54; Rum 8:23; 2Kor 5:2; 1Kor 15:51
[s]**5:5** Rum 8:23; 2Kor 1:22; Efe 1:13-14
[t]**5:6** Ebr 11:13

7 [a]kwa maana twaenenda kwa imani wala
si kwa kuona. 8 [b]Naam, tunalo tumaini na
ingekuwa bora zaidi kuuacha mwili huu na
kwenda kukaa na Bwana. 9 [c]Kwa hiyo, kama
tuko katika mwili huu au tuko mbali nao,
lengo letu ni kumpendeza Bwana. 10 [d]Kwa
kuwa sisi sote tutasimama mbele ya kiti
cha hukumu cha Kristo, ili kila mmoja
apate kulipwa kwa ajili ya yale ambayo
yametendwa katika mwili wake, yakiwa
mema au mabaya.

*Huduma Ya Upatanisho*

11 [e]Basi, kwa kuwa tunajua kumcha
Bwana, tunajitahidi kuwavuta wengine.
Lakini Mungu anatufahamu dhahiri, nami
natumaini kwamba tu dhahiri katika
dhamiri zenu pia. 12 [f]Sio kwamba tunajaribu
kujistahilisha kwenu tena, lakini tunataka
kuwapa nafasi ili mwone fahari juu yetu
mweze kuwajibu hao wanaoona fahari
juu ya mambo yanayoonekana badala ya
mambo yaliyo moyoni. 13 [g]Kama tumerukwa
na akili, ni kwa ajili ya Mungu; kama tuna
akili timamu, ni kwa ajili yenu. 14 [h]Kwa
kuwa upendo wa Kristo unatutia nguvu,
kwa sababu tunasadiki kuwa mmoja alikufa
kwa ajili ya wote, kwa hiyo wote walikufa.
15 [i]Naye alikufa kwa ajili ya watu wote,
ili kwamba wote wanaoishi wasiishi tena
kwa ajili ya nafsi zao wenyewe, bali kwa
ajili yake yeye aliyekufa na kufufuliwa tena
kwa ajili yao.

16 [j]Hivyo tangu sasa hatumwangalii mtu
yeyote kwa mtazamo wa kibinadamu.
Ingawa wakati fulani tulimwangalia Kristo
kwa namna ya kibinadamu, hatumwangalii
tena hivyo. 17 [k]Kwa hiyo kama mtu akiwa
ndani ya Kristo, amekuwa kiumbe kipya; ya
kale yamepita, tazama, yamekuwa mapya.
18 [l]Haya yote yanatokana na Mungu, ambaye
ametupatanisha sisi na nafsi yake kwa njia
ya Yesu Kristo na kutupata sisi huduma
ya upatanisho: 19 Kwamba Mungu alikuwa
ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu na
nafsi yake mwenyewe, akiwa hawahesabii
watu dhambi zao. Naye ametukabidhi sisi
ujumbe huu wa upatanisho. 20 [m]Kwa hiyo
sisi ni mabalozi wa Kristo, kana kwamba
Mungu anawasihi kupitia kwa vinywa
vyetu. Nasi twawaomba sana ninyi kwa
niaba ya Kristo, mpatanishwe na Mungu.
21 [n]Kwa maana Mungu alimfanya yeye
asiyekuwa na dhambi kuwa dhambi kwa
ajili yetu, ili sisi tupate kufanywa haki ya
Mungu kwake yeye.

6 [o]Kama watendakazi pamoja na Mungu,
tunawasihi msipokee neema ya Mungu
bure. 2 [p]Kwa maana asema:

> “Wakati wangu uliokubalika
> nilikusikia,
> siku ya wokovu nilikusaidia.”

Tazama, wakati uliokubalika ndio huu, siku
ya wokovu ndiyo sasa.

*Taabu Za Paulo*

3 [q]Hatuweki kitu cha kukwaza katika njia
ya mtu yeyote, ili huduma yetu isionekane
kuwa na lawama. 4 [r]Bali kama watumishi
wa Mungu tuonyeshe kwa kila njia: katika
saburi nyingi; katika dhiki, katika misiba,
na katika shida; 5 [s]katika kupigwa, katika
kufungwa gerezani na katika ghasia;
katika kazi ngumu, katika kukesha na

---

[a]**5:7** 1Kor 13:12; 2Kor 4:18
[b]**5:8** Yn 12:26; Flp 1:23
[c]**5:9** Rum 14:18; Efe 5:10; Kol 1:10; 1The 4:1
[d]**5:10** Mt 16:27; Mdo 10:42; Rum 2:16; 14:10; Efe 6:8
[e]**5:11** Ay 23:15; Ebr 10:31; 12:29; Yud 23; 2Kor 4:2
[f]**5:12** 2Kor 3:1; 1:14
[g]**5:13** 2Kor 11:1, 16-17; 12:11
[h]**5:14** Rum 6:6-7; Gal 2:20; Kol 3:3
[i]**5:15** Rum 14:7-9; 4:25
[j]**5:16** 2Kor 10:4; 11:18
[k]**5:17** Rum 16:3; Yn 1:13; Rum 6:4; Gal 6:15; Isa 65:17; Ufu 21:4-5
[l]**5:18** Rum 11:36; 5:10
[m]**5:20** 2Kor 6:1; Efe 6:20; Isa 27:5
[n]**5:21** Ebr 4:15; 7:26; 1Pet 2:22-24; 1Yn 3:5; Rum 1:17; 1Kor 1:30
[o]**6:1** 1Kor 3:9; 2Kor 5:20; 1Kor 15; 2
[p]**6:2** Isa 49; 8; Za 69:13; Isa 55:6
[q]**6:3** Mt 5:29; Rum 14:13-20; 1Kor 8:9-13; 9:13; 10:32
[r]**6:4** 2Kor 4:2; 1Kor 4:1
[s]**6:5** Mdo 16:23; 2Kor 11:23-25; 1Kor 4:11

katika kufunga; 6 [a]katika utakatifu, katika
ufahamu, katika uvumilivu, na katika utu
wema; katika Roho Mtakatifu na upendo
wa kweli; 7 [b]katika maneno ya kweli na
katika nguvu za Mungu, kwa silaha za
haki za mkono wa kuume na za mkono
wa kushoto; 8 [c]katika utukufu na katika
kudharauliwa; katika sifa mbaya na katika
sifa nzuri; tukiwa kama wadanganyaji,
lakini tukiwa wakweli; 9 [d]tukiwa maarufu,
lakini tukihesabiwa kama tusiojulikana;
tukiwa kama wanaokufa, lakini tunaishi;
tukipigwa, lakini hatuuawi; 10 [e]tukiwa kama
wenye huzuni, lakini siku zote tukifurahi;
tukionekana maskini, lakini tukitajirisha
wengi; tukiwa kama wasio na kitu, lakini
tuna vitu vyote.

11 [f]Tumesema nanyi wazi, enyi
Wakorintho na kuwafungulieni mioyo yetu
wazi kabisa. 12 [g]Sisi hatujizuii kuwapenda,
bali ninyi mmeuzuia upendo wenu kwetu.
13 [h]Sasa nasema, kama na watoto wangu:
Ninyi pia ifungueni mioyo yenu kabisa.

*Msifungiwe Nira Pamoja Na Wasioamini*

14 [i]Msifungiwe nira pamoja na watu
wasioamini, kwa jinsi isivyo sawasawa, kwa
maana pana uhusiano gani kati ya haki na
uovu? Au kuna ushirika gani kati ya nuru na
giza? 15 [j]Kuna mapatano gani kati ya Kristo
na Beliari?[k] Yeye aaminiye ana sehemu gani
na yeye asiyeamini? 16 [l]Kuna mapatano
gani kati ya Hekalu la Mungu na sanamu?
Kwa kuwa sisi tu Hekalu la Mungu aliye
hai. Kama Mungu alivyosema: "Nitakaa
pamoja nao na kutembea katikati yao, nami
nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu
wangu."

17 [m]"Kwa hiyo tokeni miongoni mwao,
mkatengwe nao,
asema Bwana.
Msiguse kitu chochote kilicho najisi,
nami nitawakaribisha."
18 [n]"Mimi nitakuwa Baba kwenu,
nanyi mtakuwa wanangu na binti
zangu,
asema Bwana Mwenyezi."

7 [o]Wapenzi, kwa kuwa tunazo ahadi hizi,
basi na tujitakase nafsi zetu kutokana
na kila kitu kitiacho mwili na roho unajisi,
tukitimiza utakatifu kwa kumcha Mungu.

*Furaha Ya Paulo*

2 [p]Tupatieni nafasi mioyoni mwenu.
Hatujamkosea mtu yeyote, hatujampotosha
mtu yeyote, wala hatujamdhulumu mtu
yeyote. 3 [q]Sisemi haya ili kuwahukumu, kwa
kuwa nilisema mwanzo, kwamba ninyi mko
mioyoni mwetu hata kwa kufa pamoja au
kuishi pamoja. 4 Mara nyingi najivuna kwa
ajili yenu; naona fahari juu yenu. Nimejawa
na faraja. Nina furaha kupita kiasi katika
mateso yetu yote.

5 Kwa maana hata tulipoingia Makedonia,
miili yetu haikuwa na raha. Tulisumbuliwa
kila upande, kwa nje kulikuwa na mapigano
na mioyoni mwetu tulikuwa na hofu. 6 [r]Bali
Mungu, yeye awafarijie wenye huzuni,
alitufariji kwa kufika kwake Tito. 7 Lakini
si kule kuja kwa Tito tu, bali pia kwa faraja
mliyompa. Alitueleza jinsi mlivyonionea
shauku, huzuni yenu kubwa na juhudi yenu
kwa ajili yangu, ili kwamba furaha yangu
ipate kuwa kubwa kuliko wakati wowote.

---

[a]**6:6** 1Kor 2:4; Rum 12:5; 1Tim 1:5; 1The 1:5
[b]**6:7** 2Kor 4:2-7; Rum 13:12; 2Kor 10:4; Efe 6:10-18
[c]**6:8** 1Kor 4:10-13; Mt 27:63
[d]**6:9** Rum 8:36; 2Kor 1:8-10; 4:10-11
[e]**6:10** Mt 5:12; 2Kor 7; 4; Flp 2:17; 4:4; Kol 1:24; 1The 1:6; 2Kor 8:9; Mdo 3:6; Rum 8:32
[f]**6:11** 2Kor 7:3; Za 119:32
[g]**6:12** 2Nya 12:15
[h]**6:13** 1The 2:11; 2Kor 7:2
[i]**6:14** Mwa 24:3; Kum 22:10; 1Kor 5:9-10; Efe 5:7-11
[j]**6:15** 1Kor 10:21; Mdo 5:14; 1Kor 6; 6
[k]15 Beliari hapa ina maana ya uovu, kutokumcha Mungu.
[l]**6:16** 1Kor 10:21; 3:16; Mt 16:16; Law 26:12; Yer 32:38; Eze 37:27; Ufu 21; 3
[m]**6:17** Ufu 18; 4; Isa 51:11; Eze 20:34-41
[n]**6:18** Kut 4:22; 2Sam 7:14; 1Nya 17:13; Isa 43:6; Rum 8:14; 2Sam 7:8
[o]**7:1** 2Kor 6:17-18; 1Kor 10:14; 1The 4:7; 1Pet 1:15-16
[p]**7:2** 2Kor 6:12-13
[q]**7:3** 2Kor 6:11-12; Flp 1:7
[r]**7:6** 2Kor 2:13; Za 113:6; 138:6; Isa 56:2

8 [a]Hata kama niliwahuzunisha kwa
barua yangu, sijutii. Ingawa nilijuta kwa
muda mfupi, kwa kuwa najua kwamba
barua yangu iliwaumiza, lakini ni kwa
kitambo tu, 9 lakini sasa nina furaha,
si kwa sababu mlihuzunika, bali kwa
kuwa huzuni hiyo iliwafanya mtubu.
Kwa maana mlihuzunishwa kama Mungu
alivyokusudia watu wahuzunike na hivyo
sisi hatukuwadhuru kwa njia yoyote.
10 [b]Kwa maana huzuni ya kimungu huleta
toba iletayo wokovu na wala haina majuto.
Lakini huzuni ya kidunia husababisha
mauti. 11 [c]Tazameni jinsi huzuni hii ya
kimungu ilivyoleta faida ndani yenu: bidii
mliyo nayo, juhudi mliyofanya kujitetea,
uchungu wenu, hofu yenu, upendo wenu,
shauku yenu na jinsi mlivyokuwa tayari
kutoa adhabu inayostahili. Kwa kila njia
mmejithibitisha kuwa safi katika jambo
hilo. 12 [d]Hivyo ingawa niliwaandikia,
haikuwa kwa sababu ya huyo aliyekosa
au huyo aliyekosewa. Lakini nilitaka ninyi
wenyewe mwone, mbele za Mungu, jinsi
mlivyojitoa kwa ajili yetu. 13 [e]Kwa ajili ya
haya tumefarijika.

Zaidi ya kule sisi kutiwa moyo, tulifurahi
sana kumwona Tito alivyo na furaha,
kwa sababu roho yake imeburudishwa
na ninyi nyote. 14 [f]Nilikuwa nimewasifu
ninyi kwake, nanyi hamkuniaibisha.
Lakini kila kitu tulichowaambia ninyi,
kilikuwa kweli, hivyo kule kujisifu kwetu
kwa Tito kuwahusu ninyi kumethibitishwa
kuwa kweli pia. 15 [g]Upendo wake kwenu
unaongezeka sana anapokumbuka jinsi
mlivyokuwa watiifu, na kumpokea kwa
hofu na kutetemeka. 16 [h]Nafurahi kwamba
ninaweza kuwatumaini ninyi kabisa.

[a]**7:8** 2Kor 2:2-4
[b]**7:10** Mdo 11:18
[c]**7:11** 2Kor 8:7
[d]**7:12** 2Kor 2:3; 9; 1Kor 5:1-2
[e]**7:13** 2Kor 2:13
[f]**7:14** 2Kor 8:4, 6
[g]**7:15** 2Kor 2:9; 10:6; Za 55:5; 1Kor 2:3; Flp 2:12
[h]**7:16** 2Kor 2:3

*Kutoa Kwa Ukarimu*

8 [i]Basi sasa ndugu, nataka ninyi mjue
kuhusu ile neema ambayo Mungu
amewapa makanisa ya Makedonia.
2 [j]Pamoja na majaribu makali na taabu
walizopata, furaha waliyokuwa nayo
ilikuwa kubwa, ingawa walikuwa maskini
kupindukia, kwa upande wao walifurika
kwa wingi wa ukarimu. 3 [k]Kwa maana
nashuhudia kwamba wao walitoa kwa
kadiri wawezavyo, hata na zaidi ya uwezo
wao, kwa hiari yao wenyewe, 4 [l]wakitusihi
kwa bidii wapewe fursa ya kushiriki katika
huduma hii ya kuwasaidia watakatifu.
5 Wala hawakufanya tulivyotazamia,
bali walijitoa wao wenyewe kwa Bwana
kwanza na ndipo wakajitoa kwa ajili yetu,
kufuatana na mapenzi ya Mungu. 6 [m]Kwa
hiyo tulimsihi Tito, kwa kuwa ndiye
alianzisha jambo hili, akamilishe tendo
hili la neema kwa upande wenu. 7 [n]Lakini
kama vile mlivyo mbele sana katika yote:
Katika imani, katika usemi, katika maarifa,
katika uaminifu wote na katika upendo
wenu kwetu sisi, vivyo hivyo tunataka pia
mzidi katika neema hii ya kutoa.

8 [o]Siwaamrishi, lakini nataka kujaribu
unyofu wa upendo wenu kwa kuulinganisha
na bidii ya wengine. 9 [p]Kwa maana mnajua
neema ya Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba
ingawa alikuwa tajiri, kwa ajili yenu
alikubali kuwa maskini, ili kwa umaskini
wake ninyi mpate kuwa matajiri.

10 [q]Ushauri wangu kuhusu lile lililo bora
kwenu juu ya jambo hili ni huu: Mwaka
uliopita ninyi mlikuwa wa kwanza si tu
kutoa lakini pia mlikuwa na shauku ya
kufanya hivyo. 11 [r]Sasa ikamilisheni kazi
hii kwa shauku kama mlivyoanza, jitoleeni

[i]**8:1** Mdo 16:9
[j]**8:2** Kut 36:9; 2Kor 9:11
[k]**8:3** 1Kor 16:2
[l]**8:4** Mdo 24:17; 9:13
[m]**8:6** 2Kor 12:18; 2:13
[n]**8:7** 2Kor 9:8; Rum 15:14; 1Kor 1:5; 12:8; 13:1-2; 14:6
[o]**8:8** 1Kor 7:6
[p]**8:9** Rum 3:24; 2Kor 13:14; Mt 20:28; 2Kor 6:10
[q]**8:10** 1Kor 7:25, 40; 16:2-3; 2Kor 9:2
[r]**8:11** Kut 25:2; 2Kor 9:2

kulingana na uwezo wenu. [12] [a]Kwa kuwa
kama nia ya kutoa ipo, kitolewacho
kinakubalika kulingana na kile mtu alicho
nacho, wala si kwa kile ambacho hana.
[13] Nia yetu si kwamba wengine wasaidike
wakati ninyi mnateseka, bali pawe na
uwiano. [14] [b]Kwa wakati huu, wingi wa vitu
mlivyo navyo usaidie kutosheleza mahitaji
yao, ili wakati wao watakapokuwa na wingi
wa vitu, nao wapate kutosheleza mahitaji
yenu. [15] [c]Ndipo patakuwa na usawa,
kama ilivyoandikwa: "Aliyekusanya zaidi
hakuwa na ziada, wala aliyekusanya kidogo
hakupungukiwa."

*Tito Atumwa Korintho*

[16] [d]Ninamshukuru Mungu ambaye
amemtia Tito moyo wa kuwajali ninyi kama
mimi ninavyowajali. [17] [e]Si kwamba Tito
amekubali tu ombi letu, bali anakuja kwenu
akiwa na shauku kuliko wakati mwingine,
tena kwa hiari yake mwenyewe. [18] [f]Nasi
tunamtuma pamoja naye ndugu ambaye
anasifiwa na makanisa yote kwa huduma
yake ya kuhubiri Injili. [19] [g]Zaidi ya hayo,
alichaguliwa na makanisa ili asafiri pamoja
nasi tulipokuwa tunapeleka matoleo ya
ukarimu, kwa ajili ya utukufu wa Bwana
mwenyewe, na ili kuonyesha hisani yetu
kuwasaidia. [20] Tunataka kuepuka lawama
yoyote kuhusu jinsi tunavyosimamia
matoleo haya ya ukarimu. [21] [h]Kwa kuwa
tunakusudia kufanya kile kilicho haki si
machoni mwa Bwana peke yake, bali pia
machoni mwa watu wengine.
[22] Pamoja nao, tunamtuma ndugu yetu
ambaye mara kwa mara ametuthibitishia
kwa njia nyingi kwamba ana shauku, naam,
zaidi sana sasa kwa sababu analo tumaini
kuu kwenu. [23] [i]Kwa habari ya Tito, yeye ni
mwenzangu na mtendakazi pamoja nami
miongoni mwenu. Kwa habari za ndugu
zetu, wao ni wawakilishi wa makanisa,
na utukufu kwa Kristo. [24] [j]Kwa hiyo
waonyesheni wazi hawa ndugu uthibitisho
wa upendo wenu na sababu inayotufanya
tujivune kwa ajili yenu, mbele ya makanisa,
ili yapate kuona.

*Wasaidieni Wakristo Wenzenu*

9 [k]Hakuna haja yangu kuwaandikia
kuhusu huduma hii itolewayo kwa ajili
ya watakatifu. [2] [l]Kwa kuwa ninajua mlivyo
na shauku ya kusaidia, nami nimekuwa
nikijivuna kwa ajili ya jambo hilo kwa watu
wa Makedonia, nikiwaambia kuwa ninyi wa
Akaya mmekuwa tayari kutoa tangu mwaka
jana na shauku yenu imewachochea wengi
wao katika kutoa. [3] [m]Lakini sasa nawatuma
hawa ndugu ili kujivuna kwetu kuhusu
mchango wenu kusiwe maneno matupu,
bali mpate kuwa tayari kama nilivyosema
mngekuwa tayari. [4] [n]Kwa maana kama
nikija na Mmakedonia yeyote na kuwakuta
hamjawa tayari, tutaona aibu kusema
chochote juu yenu katika matoleo. [5] [o]Kwa
hivyo niliona ni muhimu niwahimize hawa
ndugu watangulie kuja huko kwenu kabla
yangu, wafanye mipango ya hayo matoleo
ya ukarimu mliyokuwa mmeahidi, ili yawe
tayari kama matoleo ya hiari wala si kama
ya kutozwa kwa nguvu.

*Kupanda Kwa Ukarimu*

[6] [p]Kumbukeni kwamba: Yeyote apandaye
kwa uchache pia atavuna kwa uchache,
naye apandaye kwa ukarimu pia atavuna
kwa ukarimu. [7] [q]Kila mtu atoe kama
anavyokusudia moyoni mwake, si kwa
uchoyo au kwa kulazimishwa, kwa maana
Mungu humpenda yeye atoaye kwa moyo

---

[a]**8:12** Mk 12:43, 44; 2Kor 9:7
[b]**8:14** Mdo 4:34; 2Kor 9:12
[c]**8:15** Kut 16:18
[d]**8:16** 2Kor 2:14; Ufu 17:17; 2Kor 2:13
[e]**8:17** 2Kor 8:6
[f]**8:18** 2Kor 12:18; 1Kor 7:17; 2Kor 2:12
[g]**8:19** Mdo 14:23; 1Kor 16:3-4
[h]**8:21** Rum 12:17; 14:18; Tit 2:14-15
[i]**8:23** 2Kor 2:13; Flp 1:17; 2:25
[j]**8:24** 2Kor 7:4, 14; 9:2
[k]**9:1** 1The 4:9; Mdo 24; 17; 9:13
[l]**9:2** 2Kor 8:11-19; 7:4, 14; 8:10, 24; Mdo 18:12
[m]**9:3** 2Kor 8:23; 1Kor 16:2
[n]**9:4** Rum 15:26
[o]**9:5** Flp 4:17; 2Kor 12:17-18
[p]**9:6** Mit 11:24-25; 22:9; Gal 6:7-9
[q]**9:7** Kut 25:2; 2Kor 8:12; Kum 15:10; Rum 12:8

mkunjufu. 8 [a]Naye Mungu aweza kuwapa
kila baraka kwa wingi, ili katika mambo yote
kila wakati, mwe na kila kitu mnachohitaji,
ili mweze kushiriki kwa wingi katika kila
kazi njema. 9 [b]Kama ilivyoandikwa:

“Ametawanya vipawa vyake kwa
ukarimu
akawapa maskini;
haki yake hudumu milele.”

10 [c]Yeye ampaye mpanzi mbegu kwa ajili
ya kupanda na mkate kuwa chakula,
atawapa na kuzizidisha mbegu zenu za
kupanda na kuongeza mavuno ya haki
yenu. 11 [d]Mtatajirishwa kwa kila namna
ili mpate kuwa wakarimu kila wakati, na
kupitia kwetu, ukarimu wenu utamletea
Mungu shukrani.
12 [e]Huduma hii mnayofanya si tu kwa
ajili ya kukidhi mahitaji ya watakatifu,
bali huzidi sana kwa shukrani nyingi
apewazo Mungu. 13 Kwa sababu ya huduma
ambayo mmejithibitisha wenyewe, watu
watamtukuza Mungu kwa ajili ya utiifu
ufuatanao na ukiri wenu wa Injili ya Kristo,
na kwa ukarimu wenu wa kushiriki pamoja
nao na pia wengine wote. 14 [f]Nao katika
maombi yao kwenu mioyo yao itawaonea
shauku kwa sababu ya neema ipitayo kiasi
mliyopewa na Mungu. 15 [g]Ashukuriwe
Mungu kwa karama yake isiyoelezeka.

*Paulo Atetea Huduma Yake*

10 [h]Basi, mimi Paulo ninawasihi kwa
unyenyekevu na upole wa Kristo, mimi
niliye “mwoga” ninapokuwa pamoja nanyi
ana kwa ana, lakini mwenye ujasiri nikiwa
mbali nanyi! 2 [i]Nawaomba nitakapokuja
kwenu nisiwe na ujasiri dhidi ya watu
fulani, kama ninavyotazamia kwa wale
wanaodhani kwamba tunaishi kwa kufuata
namna ya ulimwengu huu. 3 [j]Ingawa tunaishi
duniani, hatupigani vita kama ulimwengu
ufanyavyo. 4 [k]Silaha za vita vyetu si za
mwili, bali zina uwezo katika Mungu hata
kuangusha ngome, 5 [l]tukiangusha mawazo
na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu
ya elimu ya Mungu, na tukiteka nyara kila
fikira ipate kumtii Kristo, 6 [m]tena tukiwa
tayari kuadhibu kila tendo la kutotii, kutii
kwenu kutakapokamilika.
7 [n]Angalieni yale yaliyo machoni penu.
Kama mtu yeyote anaamini kuwa yeye
ni mali ya Kristo, basi kumbuka kuwa
kama ulivyo wa Kristo, vivyo hivyo na
sisi ndivyo tulivyo. 8 [o]Basi hata kama
nikijisifu zaidi kidogo kuhusu mamlaka
tuliyo nayo, ambayo Bwana alitupa ili
kuwajenga wala si kuwabomoa, mimi
sitaionea haya. 9 [p]Sitaki nionekane kama
ninayejaribu kuwatisha kwa nyaraka zangu.
10 [q]Kwa maana wanasema, “Nyaraka zake ni
nzito na zenye nguvu, lakini ana kwa ana
ni dhaifu na kuzungumza kwake ni kwa
kudharauliwa.” 11 [r]Watu kama hao wajue
ya kuwa, yale tusemayo kwa barua tukiwa
hatupo pamoja nanyi, ndivyo tulivyo na
ndivyo tutakavyofanya tutakapokuwa
pamoja nanyi.
12 [s]Hatuthubutu kujiweka kwenye kundi
moja au kujilinganisha na hao wanaojitukuza
wenyewe kuwa wao ni wa maana sana.
Wanapojipima na kujilinganisha wenyewe
kwa wenyewe, wanaonyesha ya kuwa
hawana busara. 13 [t]Lakini sisi hatujajivuna
kupita kiasi, bali majivuno yetu yatakuwa
katika mipaka ile Mungu aliyotuwekea,
mipaka ambayo inawafikia hata ninyi.

[a]**9:8** Efe 3:20; Flp 4:19
[b]**9:9** Mal 3:10; Za 112:9
[c]**9:10** Isa 55:10; Hos 10:12
[d]**9:11** 1Kor 1:5; 2Kor 1:11; 4:15
[e]**9:12** 2Kor 8:12; 1:11
[f]**9:14** 2Kor 8:1
[g]**9:15** 2Kor 2:14; Rum 5:15-16
[h]**10:1** Mt 11:29; Gal 5:2; Efe 3:1
[i]**10:2** 1Kor 4:21; Rum 12:2
[j]**10:3** 2Kor 10:2
[k]**10:4** 2Kor 6:7; Yer 1:10; 2Kor 13:10
[l]**10:5** Isa 2:10-12; 1Kor 1:19; 2Kor 9:13
[m]**10:6** 2Kor 6:9; 7:15
[n]**10:7** Yn 7:24; 2Kor 5:12; 1Kor 1:12; 3:23; 14:37; 2Kor 11:23
[o]**10:8** Yer 1:10; 2Kor 13:10
[p]**10:9** 1Kor 2:3; Gal 4:13-14; 1Kor 1:17; 2Kor 11:6
[q]**10:10** 1Kor 2:3; Gal 4:13-14; 1Kor 1:17; 2Kor 11:6
[r]**10:11** 2Kor 13:2, 10
[s]**10:12** 2Kor 3:1
[t]**10:13** Rum 12:3

[14] [a]Kwa maana hatukuwa tunavuka mipaka
katika kujisifu kwetu, kama vile ambavyo
ingekuwa kama hatukuwa tumekuja
kwenu. Kwa maana sisi ndio tuliokuwa
wa kwanza kuja kwenu na Injili ya Kristo.
[15] [b]Wala hatuvuki mipaka kwa kujisifu
kwetu kwa ajili ya kazi iliyofanywa na
watu wengine. Tumaini letu ni kwamba
imani yenu inavyozidi kukua, eneo letu
la utendaji miongoni mwenu litapanuka
zaidi, [16] [c]ili tuweze kuhubiri Injili sehemu
zilizo mbali na maeneo yenu. Kwa maana
hatutaki kujisifu kwa ajili ya kazi ambayo
imekwisha kufanyika tayari katika eneo la
mtu mwingine. [17] [d]Lakini, “Yeye ajisifuye
na ajisifu katika Bwana.” [18] [e]Kwa maana si
yeye ajisifuye mwenyewe akubaliwaye, bali
yeye ambaye Bwana humsifu.

*Paulo Na Mitume Wa Uongo*

11 [f]Laiti mngenivumilia kidogo katika
upumbavu wangu! Naam, nivumilieni
kidogo. [2] [g]Ninawaonea wivu, wivu wa
Kimungu, kwa kuwa mimi niliwaposea
mume mmoja, ili niwalete kwa Kristo
kama mabikira safi. [3] [h]Lakini nina hofu
kuwa, kama vile Eva alivyodanganywa kwa
ujanja wa yule nyoka, mawazo yenu yasije
yakapotoshwa, mkauacha unyofu na usafi
wa upendo wenu kwa Kristo. [4] [i]Kwa sababu
kama mtu akija na kuwahubiria Yesu
mwingine ambaye si yule tuliyemhubiri,
au kama mkipokea roho mwingine ambaye
si yule mliyempokea, au Injili tofauti
na ile mliyoikubali, ninyi mnaitii kwa
urahisi. [5] [j]Lakini sidhani ya kuwa mimi ni
dhalili sana kuliko hao “mitume wakuu.”
[6] [k]Inawezekana mimi nikawa si mnenaji
hodari, lakini ni hodari katika elimu. Jambo
hili tumelifanya liwe dhahiri kwenu kwa
njia zote.
[7] [l]Je, nilitenda dhambi kwa kujishusha ili
kuwainua ninyi kwa kuwahubiria Injili ya
Mungu pasipo malipo? [8] [m]Niliyanyang’anya
makanisa mengine kwa kupokea misaada
kutoka kwao ili niweze kuwahudumia
ninyi. [9] [n]Nami nilipokuwa pamoja nanyi,
nikipungukiwa na chochote, sikuwa
mzigo kwa mtu yeyote, kwa maana ndugu
waliotoka Makedonia walinipatia mahitaji
yangu. Kwa hiyo nilijizuia kuwa mzigo
kwenu kwa njia yoyote, nami nitaendelea
kujizuia. [10] [o]Kwa hakika kama vile kweli
ya Kristo ilivyo ndani yangu, hakuna mtu
yeyote katika Akaya nzima atakayenizuia
kujivunia jambo hili. [11] [p]Kwa nini? Je, ni
kwa sababu siwapendi? Mungu anajua ya
kuwa nawapenda! [12] [q]Nami nitaendelea
kufanya lile ninalofanya sasa ili nisiwape
nafasi wale ambao wanatafuta nafasi ya
kuhesabiwa kuwa sawa na sisi katika
mambo wanayojisifia.
[13] [r]Watu kama hao ni mitume wa
uongo, ni wafanyakazi wadanganyifu,
wanaojigeuza waonekane kama mitume wa
Kristo. [14] [s]Wala hii si ajabu, kwa kuwa hata
Shetani mwenyewe hujigeuza aonekane
kama malaika wa nuru. [15] [t]Kwa hiyo basi
si ajabu, kama watumishi wa Shetani nao
hujigeuza ili waonekane kama watumishi
wa haki. Mwisho wao utakuwa sawa na
matendo yao yanavyostahili.

*Paulo Anajivunia Mateso Yake*

[16] [u]Nasema tena, mtu yeyote asidhani
kwamba mimi ni mjinga. Lakini hata
kama mkinidhania hivyo, basi nipokeeni
kama mjinga ili nipate kujisifu kidogo.

---

[a]**10:14** 1Kor 3:6; 2Kor 2:12
[b]**10:15** Rum 15:20; 2The 1:3
[c]**10:16** Rum 1:1; 2Kor 2:12; Mdo 19:21
[d]**10:17** Yer 9:24; Za 34:2; 44:8; 1Kor 1:31
[e]**10:18** Rum 2:29
[f]**11:1** Mt 17:17; 2Kor 5:13
[g]**11:2** Hos 2:19; Efe 5:26-27
[h]**11:3** Mwa 3:1-6; 1Tim 2:14; Ufu 12:5
[i]**11:4** 1Kor 3:11; Rum 8:15; Gal 1:6-9
[j]**11:5** 2Kor 12:11; Gal 2:6
[k]**11:6** 1Kor 1:17; 2Kor 9:7; Efe 3:4
[l]**11:7** 2Kor 12:13; Rum 1:1; 1Kor 9:18
[m]**11:8** Flp 4:15-18
[n]**11:9** Flp 4:15; 2Kor 12:13-16
[o]**11:10** Rum 9:1; Mdo 18:12; 1Kor 9:15
[p]**11:11** Rum 1:9; 2Kor 12:15
[q]**11:12** 2Kor 9:12
[r]**11:13** Mt 7:15; Tit 1:10; Ufu 2:2
[s]**11:14** Mt 4:10
[t]**11:15** Mt 16:27; Flp 3:19
[u]**11:16** 2Kor 11:1; 12:6, 11

17 [a]Ninayosema kuhusiana na huku
kujisifu kwa kujiamini, sisemi kama vile
ambavyo Bwana angesema, bali kama
mjinga. 18 [b]Kwa kuwa wengi wanajisifu
kama vile ulimwengu ufanyavyo, mimi
nami nitajisifu. 19 [c]Ninyi mwachukuliana
na wajinga kwa sababu mna hekima sana!
20 [d]Kweli ni kwamba mnachukuliana na mtu
akiwatia utumwani au akiwatumia kwa ajili
ya kupata faida au akiwanyang'anya au
akijitukuza mwenyewe au akiwadanganya.
21 [e]Kwa aibu inanipasa niseme kwamba sisi
tulikuwa dhaifu sana kwa jambo hilo!

Lakini chochote ambacho mtu mwingine
yeyote angethubutu kujisifia, nanena
kama mjinga, nami nathubutu kujisifu juu
ya hilo. 22 [f]Je, wao ni Waebrania? Mimi
pia ni Mwebrania. Je, wao ni Waisraeli?
Mimi pia ni Mwisraeli. Je, wao ni wazao
wa Abrahamu? Mimi pia ni mzao wa
Abrahamu. 23 [g]Je, wao ni watumishi wa
Kristo? (Nanena kiwazimu.) Mimi ni zaidi
yao. Nimefanya kazi kwa bidii kuwaliko
wao, nimefungwa gerezani mara kwa
mara, nimechapwa mijeledi sana, na
nimekabiliwa na mauti mara nyingi.
24 [h]Mara tano nimechapwa na Wayahudi
viboko arobaini kasoro kimoja. 25 [i]Mara tatu
nilichapwa kwa fimbo, mara moja nilipigwa
kwa mawe, mara tatu nimevunjikiwa na
meli, nimekaa kilindini usiku kucha na
mchana kutwa, 26 [j]katika safari za mara kwa
mara. Nimekabiliwa na hatari za kwenye
mito, hatari za wanyang'anyi, hatari kutoka
kwa watu wangu mwenyewe, hatari kutoka
kwa watu wa Mataifa; hatari mijini, hatari
nyikani, hatari baharini; na hatari kutoka
kwa ndugu wa uongo. 27 [k]Nimekuwa katika
kazi ngumu na taabu, katika kukesha mara
nyingi; ninajua kukaa njaa na kuona kiu;
nimefunga kula chakula mara nyingi;
nimehisi baridi na kuwa uchi. 28 [l]Zaidi ya
hayo yote, nakabiliwa na mzigo wa wajibu
wangu kwa makanisa yote. 29 [m]Je, ni nani
aliye mdhaifu, nami nisijisikie mdhaifu? Je,
nani aliyekwazwa, nami nisiudhike?

30 [n]Kama ni lazima nijisifu, basi nitajisifia
yale mambo yanayoonyesha udhaifu wangu.
31 [o]Mungu na Baba wa Bwana Yesu, yeye
ambaye anahimidiwa milele, anajua ya
kuwa mimi sisemi uongo. 32 [p]Huko Dameski,
mtawala aliyekuwa chini ya Mfalme Areta
aliulinda mji wa Dameski ili kunikamata.
33 Lakini nilishushwa kwa kapu kubwa
kupitia katika dirisha ukutani, nikatoroka
kutoka mikononi mwake.

*Maono Ya Paulo Na Mwiba Aliokuwa Nao*

12 [q]Yanipasa nijisifu, ingawa haifaidi kitu.
Nitaenda kwenye maono na ufunuo
kutoka kwa Bwana. 2 [r]Namjua mtu mmoja
katika Kristo ambaye miaka kumi na minne
iliyopita alichukuliwa juu hadi mbingu ya
tatu. Kama ni katika mwili au nje ya mwili,
sijui, Mungu ajua. 3 Nami najua ya kwamba
mtu huyu, kwamba ni katika mwili au nje
ya mwili mimi sijui, lakini Mungu ajua,
4 [s]alinyakuliwa hadi Paradiso.[t] Huko alisikia
mambo yasiyoelezeka, mambo ambayo
binadamu hana ruhusa ya kuyasimulia.
5 [u]Nitajisifu kwa ajili ya mtu kama huyo,
lakini sitajisifu kuhusu mimi mwenyewe
ila mimi nitajisifia udhaifu wangu. 6 [v]Hata
kama ningependa kujisifu, sitakuwa mjinga,
kwa maana nitakuwa nasema kweli. Lakini
najizuia, ili mtu yeyote asije akaniona mimi

[a]**11:17** 1Kor 7:12, 25; 2Kor 11:21; 1Kor 7:6
[b]**11:18** 2Kor 5:16; 10:4; Flp 3:3-4
[c]**11:19** 1Kor 4:10; 2Kor 11:1
[d]**11:20** 2Kor 11:1
[e]**11:21** 2Kor 10:1; Flp 3:4
[f]**11:22** Flp 3:5; Rum 9:4; 11:1; Lk 3:8
[g]**11:23** 1Kor 3:5; 15:10; Mdo 16:23; 2Kor 6:4-5; Rum 8:36
[h]**11:24** Kum 25:3
[i]**11:25** Mdo 16:22; 14:19; 27:1-44
[j]**11:26** Mdo 20:3; 21:31; Gal 2:4
[k]**11:27** Mdo 18:3; Kol 1:29; 1Kor 4:11-12; 2Kor 6:5
[l]**11:28** 1Kor 7:17
[m]**11:29** Rum 14:1; 1Kor 2:3; Mt 5:29
[n]**11:30** Gal 6:14; 2Kor 12:5-9; 1Kor 2:3
[o]**11:31** Rum 1:25; 9:5
[p]**11:32** Mdo 9:24; 9:25
[q]**12:1** 2Kor 11:16; 1Kor 2:10
[r]**12:2** Rum 16:3; Mdo 8:39; Efe 4:10; 2Kor 11:11
[s]**12:4** Lk 23:43; Ufu 2:7; 12; 5; 1Kor 2:3
[t]4 Paradiso hapa ina maana mbinguni.
[u]**12:5** 1Kor 2:3; 2Kor 11:9, 10, 30
[v]**12:6** 2Kor 10:8; 11:16

kuwa bora zaidi kuliko ninavyoonekana
katika yale ninayotenda na kusema.
[7] [a]Ili kunizuia nisijivune kwa sababu
ya ufunuo huu mkuu, nilipewa mwiba
katika mwili wangu, mjumbe wa Shetani,
ili anitese. [8] [b]Kwa habari ya jambo hili
nilimsihi Bwana mara tatu aniondolee
mwiba huu. [9] [c]Lakini aliniambia, “Neema
yangu inakutosha, kwa kuwa uweza wangu
hukamilika katika udhaifu.” Kwa hiyo
nitajisifu kwa furaha zaidi kuhusu udhaifu
wangu, ili uweza wa Kristo ukae juu yangu.
[10] [d]Hii ndiyo sababu, kwa ajili ya Kristo,
nafurahia udhaifu, katika kutukanwa,
katika taabu, katika mateso na katika shida,
kwa maana ninapokuwa dhaifu, ndipo nina
nguvu.

*Wasiwasi Wa Paulo Kwa Wakorintho*

[11] [e]Nimekuwa mjinga, lakini ninyi
mmenilazimisha niwe hivyo. Kwa kuwa
ilinipasa kusifiwa na ninyi, kwa sababu
mimi si dhalili kuliko wale “mitume walio
bora,” ingawa mimi si kitu. [12] [f]Mambo
yanayomtambulisha mtume wa kweli, yaani,
ishara, miujiza na maajabu, yalifanywa
miongoni mwenu kwa saburi nyingi. [13] [g]Je,
ninyi ni kitu gani mlichopungukiwa kuliko
makanisa mengine, ila tu kwamba mimi
sikuwa mzigo kwenu? Nisameheni kwa
kosa hili!
[14] [h]Sasa niko tayari kuja kwenu kwa
mara hii ya tatu, nami sitawalemea,
kwa sababu sitahitaji chochote chenu,
ila ninawahitaji ninyi, kwa kuwa hata
hivyo watoto hawaweki akiba kwa ajili ya
wazazi wao, bali wazazi huweka akiba kwa
ajili ya watoto wao. [15] [i]Hivyo nitafurahi
kutumia kila kitu nilicho nacho kwa ajili
yenu, hata mwili wangu pia. Hata ingawa
inaonekana ninavyozidi kuwapenda, ndivyo
upendo wenu kwangu unavyopungua.
[16] [j]Iwe iwavyo, kwa vyovyote vile mimi
sikuwalemea. Lakini kwa mimi kuwa
mwerevu naliwapata. [17] [k]Je, nilijipatia faida
kwa kumtumia mtu yeyote niliyemtuma
kwenu? [18] [l]Nilimshawishi Tito aje kwenu,
nami nilimtuma pamoja na ndugu yetu. Je,
Tito aliwatumia ninyi ili kujipatia faida? Je,
hatuenendi kwa roho moja, na hatuchukui
hatua zile zile?
[19] [m]Je, mmekuwa mkifikiri kwamba
sisi tunajaribu kujitetea mbele yenu? Sisi
tumekuwa tukinena mbele za Mungu kama
wale walio katika Kristo. Na chochote
tufanyacho, ndugu wapendwa, ni kwa ajili
ya kuwatia nguvu. [20] [n]Kwa kuwa nina hofu
ya kwamba nitakapokuja naweza kuwakuta
nisivyotaka, nanyi mkanikuta msivyotaka.
Nina hofu kwamba panaweza kuwa na
ugomvi, wivu, ghadhabu, fitina, masingizio,
masengenyo, majivuno na machafuko.
[21] [o]Nina hofu kwamba nitakapokuja tena
kwenu, Mungu wangu atanidhili mbele
yenu, nami nitasikitishwa na wengi
waliotenda dhambi mbeleni, na wala
hawajatubu kwa uchafu wao, uasherati,
na ufisadi walioushiriki.

*Maonyo Ya Mwisho*

13 [p]Hii ndiyo mara ya tatu mimi
kuja kwenu. “Shtaka lolote lazima
lithibitishwe na mashahidi wawili au
watatu.” [2] [q]Nimekwisha kuwaonya
nilipokuwa pamoja nanyi mara ya pili. Sasa
narudia wakati sipo, kwamba nikija tena
sitawahurumia wale waliokuwa wametenda
dhambi hapo awali na wengine wote, [3] [r]kwa
kuwa mnadai uthibitisho kwamba Kristo
anazungumza kwa kunitumia mimi. Yeye si

[a]**12:7** 1Kor 2:10; Hes 33:55; Mt 4:10
[b]**12:8** Mt 26:39, 44
[c]**12:9** Rum 3:24; Flp 4:13; 1Fal 19:12
[d]**12:10** Mt 5:12; 2Kor 6:4; 2The 1:4; 2Kor 13:4
[e]**12:11** 2Kor 11:1-5; 1Kor 15:9-10
[f]**12:12** Yn 4:48
[g]**12:13** 1Kor 9:12, 18; 2Kor 11:7
[h]**12:14** 2Kor 13:1; 1Kor 4:14-15; Mit 19:14
[i]**12:15** Flp 2:17; 1The 2:8; 2Kor 11:11
[j]**12:16** 2Kor 11:9
[k]**12:17** 2Nya 7:12
[l]**12:18** 2Kor 8:6, 16; 2:13; 10:8
[m]**12:19** Rum 9:1; 14:19; 1Kor 10:14; 2Kor 10:8
[n]**12:20** 2Kor 2:1-4; 1Kor 4:21; Gal 5:20; Rum 1:30; 1:29
[o]**12:21** 2Kor 2:14; 13:2
[p]**13:1** 2Kor 12:14; Kum 19:15; Mt 18:16
[q]**13:2** 2Kor 1:23; 12:21
[r]**13:3** Mt 10:20; 1Kor 5:4

dhaifu katika kushughulika nanyi, bali ana
nguvu kati yenu. 4 [a]Kwa kuwa alisulubiwa
katika udhaifu, lakini anaishi kwa nguvu za
Mungu. Vivyo hivyo, sisi tu dhaifu kupitia
kwake, lakini katika kuwashughulikia ninyi
tutaishi pamoja naye kwa nguvu za Mungu.
5 [b]Jichunguzeni wenyewe mwone kama
mnaishi katika imani. Jipimeni wenyewe.
Je, hamtambui ya kuwa Yesu Kristo yumo
ndani yenu? Kama sivyo, basi, mmeshindwa
kufikia kipimo hicho! 6 Natumaini mtaona
kuwa sisi hatukushindwa. 7 [c]Lakini
tunamwomba Mungu msije mkatenda kosa
lolote, si ili sisi tuonekane kuwa tumeshinda
hilo jaribio, bali ili ninyi mtende lililo haki,
hata kama tutaonekana kuwa tumeshindwa.
8 [d]Kwa maana hatuwezi kufanya lolote
kinyume na kweli, bali kuithibitisha
kweli tu. 9 [e]Tunafurahi wakati wowote sisi
tunapokuwa dhaifu, lakini ninyi mkawa
na nguvu. Nayo maombi yetu ni kwamba
mpate kuwa wakamilifu. 10 [f]Hii ndiyo
sababu nawaandikia mambo haya wakati
sipo, ili nikija nisiwe mkali katika kutumia
mamlaka yangu, mamlaka Bwana aliyonipa
ya kuwajenga ninyi wala si ya kuwabomoa.

### *Salamu Za Mwisho*

11 [g]Hatimaye, ndugu zangu, kwaherini.
Kuweni wakamilifu, mkafarijike, kuweni wa
nia moja, kaeni kwa amani. Naye Mungu wa
upendo na amani atakuwa pamoja nanyi.
12 [h]Salimianeni ninyi kwa ninyi kwa busu
takatifu. 13 [i]Watakatifu wote wanawasalimu.
14 [j]Neema ya Bwana Yesu Kristo, na
upendo wa Mungu, na ushirika wa Roho
Mtakatifu ukae nanyi nyote. Amen.

---

[a]**13:4** 1Kor 1:25; 1Pet 3:18; Rum 1:4; 6:4; 1Kor 6:14
[b]**13:5** 1Kor 11:28; Yn 6:6; Rum 8:10
[c]**13:7** 2Kor 6:9
[d]**13:8** 1Kor 13:6
[e]**13:9** 1Kor 2:3; 2Kor 4:12; Efe 4:13
[f]**13:10** 2Kor 1:23; 10:8
[g]**13:11** 1The 4:1; 2The 3:1; Mk 9:50; 1Yn 4:16; Rum 15:33; Efe 6:23
[h]**13:12** Rum 16:16; 1Kor 16:20; 1The 5:26
[i]**13:13** Flp 4:22
[j]**13:14** Rum 16:20; 2Kor 8:9; Rum 5:5; Yud 21; Flp 2:1

# WAGALATIA

*Salamu*

1 [a]Paulo mtume: si mtume wa wanadamu
wala aliyetumwa na mwanadamu, bali
na Yesu Kristo na Mungu Baba aliyemfufua
Yesu kutoka kwa wafu; 2 [b]na ndugu wote
walio pamoja nami:
Kwa makanisa ya Galatia:
3 [c]Neema iwe nanyi na amani itokayo kwa
Mungu Baba yetu na kwa Bwana wetu Yesu
Kristo, 4 [d]aliyejitoa kwa ajili ya dhambi zetu
ili apate kutuokoa katika ulimwengu huu
wa sasa ulio mbaya, sawasawa na mapenzi
yake yeye aliye Mungu na Baba yetu.
5 [e]Utukufu una yeye milele na milele. Amen.

*Hakuna Injili Nyingine*

6 [f]Nashangaa kwamba mnamwacha
upesi hivyo yeye aliyewaita kwa neema
ya Kristo na kuifuata Injili nyingine,
7 [g]ambayo kwa kweli si Injili kamwe, ila
kwa dhahiri kuna watu wanaowachanganya
na wanaotaka kuipotosha Injili ya Kristo.
8 [h]Lakini hata ikiwa sisi au malaika atokaye
mbinguni akihubiri Injili nyingine tofauti
na ile tuliyowahubiria sisi, basi mtu huyo
alaaniwe milele! 9 [i]Kama vile tulivyokwisha
kusema kabla, sasa nasema tena, ikiwa mtu
yeyote atawahubiria Injili kinyume na ile
mliyoipokea na alaaniwe milele!
10 [j]Je, sasa mimi ninatafuta kukubaliwa
na wanadamu au kukubaliwa na Mungu?
Au nataka kuwapendeza wanadamu? Kama
ningekuwa bado najaribu kuwapendeza
wanadamu, nisingekuwa mtumishi wa
Kristo.

*Paulo Ameitwa Na Mungu*

11 [k]Ndugu zangu, nataka mjue kwamba
Injili niliyowahubiria haikutokana na
wanadamu. 12 [l]Kwa maana mimi sikuipokea
hiyo Injili kutoka kwa mwanadamu, wala
sikufundishwa na mtu, bali niliipata kwa
ufunuo kutoka kwa Yesu Kristo.
13 [m]Ninyi mmekwisha kusikia juu ya
maisha yangu ya zamani nilipokuwa
katika dini ya Kiyahudi, jinsi nilivyolitesa
kanisa la Mungu kwa nguvu na kujaribu
kuliangamiza. 14 [n]Nami niliendelea sana
katika dini ya Kiyahudi kuliko Wayahudi
wengi wa rika yangu maana nilijitahidi
sana katika desturi za baba zangu. 15 [o]Lakini
ilipompendeza Mungu, aliyenitenga tangu
tumboni mwa mama yangu na kuniita kwa
neema yake, 16 [p]alimdhihirisha Mwanawe
kwangu, ili nipate kumhubiri miongoni
mwa watu wa Mataifa. Mimi sikushauriana
na mwanadamu yeyote, 17 [q]wala sikupanda
kwenda Yerusalemu kuwaona hao
waliokuwa mitume kabla yangu, bali
nilikwenda mara moja Arabuni na kisha
nikarudi Dameski.
18 [r]Kisha baada ya miaka mitatu nilipanda
kwenda Yerusalemu kuonana na Kefa[s] na
nilikaa naye siku kumi na tano. 19 [t]Lakini
sikumwona mtume mwingine yeyote
isipokuwa Yakobo, ndugu yake Bwana.
20 [u]Nawahakikishia mbele za Mungu kuwa
ninayowaandikia si uongo. 21 [v]Baadaye

[a]**1:1** Mdo 9:15; 20:24; 1Kor 1:1
[b]**1:2** Flp 4:21; Mdo 16:6; 1Kor 16:1
[c]**1:3** Rum 1:7; 1Kor 1:3; 2Kor 1:2; Efe 1:2; Flp 1:2; Kol 1:2; 1The 1:1
[d]**1:4** Rum 4:25; 1Kor 15:3; Flp 4:20
[e]**1:5** Rum 11:36
[f]**1:6** Gal 5:8; 2Kor 11:4
[g]**1:7** Mdo 15:24; Gal 5:10
[h]**1:8** 2Kor 11:4; Rum 9:3
[i]**1:9** Rum 16:17; Kum 4:2; 12:32; Mit 30:6; Ufu 22:18
[j]**1:10** 1The 2:4; 1Sam 24:7; Mt 28:14; 1Yn 3:9; 1The 2:4
[k]**1:11** 1Kor 15:1
[l]**1:12** 1Kor 15:1, 3; Gal 1:1; Efe 3:3
[m]**1:13** Mdo 26:4, 5; 8:3
[n]**1:14** Mt 15:2
[o]**1:15** Isa 49:1, 5; Mdo 9:15
[p]**1:16** Gal 2:9; Mt 16:17
[q]**1:17** Mdo 9:2, 19-22
[r]**1:18** Mdo 9:22, 23; 9:26, 27
[s]18 Yaani Petro.
[t]**1:19** Mt 13:55
[u]**1:20** Rum 9:1; 1:9
[v]**1:21** Mdo 6:9; 9:30

nilikwenda sehemu za Syria[a] na Kilikia.
22 [b]Lakini mimi binafsi sikujulikana kwa
makanisa ya huko Uyahudi yaliyo katika
Kristo. 23 [c]Wao walisikia habari tu kwamba,
"Mtu yule ambaye hapo kwanza alikuwa
akitutesa sasa anahubiri imani ile ile
aliyokuwa akijaribu kuiangamiza." 24 [d]Nao
wakamtukuza Mungu kwa sababu yangu.

*Paulo Akubaliwa Na Mitume*

2 [e]Kisha, baada ya miaka kumi na minne,
nilipanda tena kwenda Yerusalemu
pamoja na Barnaba, nikamchukua na
Tito ili awe pamoja nami. 2 [f]Nilikwenda
kwa sababu nilikuwa nimefunuliwa na
Mungu, ili nikawaeleze kwa faragha wale
walioonekana kuwa viongozi, ile Injili
ninayoihubiri kwa watu wa Mataifa.
Nilifanya hivyo kwa kuhofia kwamba nisije
nikawa nilikuwa ninakimbia au nilikimbia
bure. 3 [g]Lakini hata Tito ambaye alikuwa
Myunani, hakulazimika kutahiriwa.
4 [h]Lakini kwa sababu ya ndugu wa uongo
ambao walijiingiza kwa siri katikati yetu
ili kupeleleza uhuru wetu tulio nao katika
Kristo Yesu, wapate kututia utumwani,
5 [i]hatukukubaliana nao hata dakika moja,
ili kwamba ukweli wa Injili ubaki nanyi.

6 [j]Kwa habari ya wale waliokuwa
wakubaliwe kuwa viongozi (kwangu mimi
sikujali vyeo vyao, maana Mungu hana
upendeleo), wale watu hawakuniongezea
chochote. 7 [k]Badala yake walitambua
kwamba nilikuwa nimekabidhiwa kazi
ya kuhubiri Injili kwa watu wa Mataifa,
kama vile Petro alivyokabidhiwa kuhubiri
Injili kwa Wayahudi. 8 [l]Kwa maana, Mungu
aliyekuwa akitenda kazi katika huduma
ya Petro kama mtume kwa Wayahudi,
ndiye pia aliyekuwa anatenda kazi katika
huduma yangu kama mtume kwa watu
wa Mataifa. 9 [m]Basi, Yakobo, Kefa[n] na
Yohana, walioonekana kama nguzo za
kanisa, walitupa mkono wa shirika, mimi
na Barnaba walipotambua ile neema
niliyopewa. Wakakubali kwamba sisi
twende kwa watu wa Mataifa na wao
waende kwa Wayahudi. 10 [o]Walichotuomba
ni kwamba tuendelee kuwakumbuka
maskini, jambo ambalo ndilo nililokuwa
na shauku ya kulifanya.

*Paulo Ampinga Petro Huko Antiokia*

11 [p]Lakini Petro alipofika Antiokia, mimi
nilimpinga ana kwa ana kwa sababu
alikuwa amekosea kwa wazi. 12 [q]Kabla
baadhi ya watu waliotoka kwa Yakobo
hawajafika, alikuwa akila pamoja na watu
wa Mataifa. Lakini hao watu walipofika
alianza kujiondoa na kujitenga na watu wa
Mataifa kwa sababu aliwaogopa wale wa
kundi la tohara. 13 [r]Pia Wayahudi wengine
waliungana naye katika unafiki huu, hata
Barnaba naye akapotoshwa na unafiki wao.

14 [s]Nilipoona kwamba hawatendi
sawasawa na kweli ya Injili, nilimwambia
Petro mbele ya wote, "Wewe ni Myahudi,
nawe unaishi kama mtu wa Mataifa na
wala si kama Myahudi. Imekuwaje basi,
mnawalazimisha watu wa Mataifa kufuata
desturi za Kiyahudi?

*Wayahudi Na Watu Wa Mataifa Wanaokolewa Kwa Imani*

15 [t]"Sisi wenyewe ni Wayahudi kwa
kuzaliwa na si watu wenye dhambi kama

---

[a]21 Syria hapa ina maana ya Shamu.
[b]**1:22** 1The 2:14; Rum 16:3
[c]**1:23** Mdo 6:7; 8:3
[d]**1:24** Mt 9:8
[e]**2:1** Mdo 15:2; 4:36; 2Kor 2:13
[f]**2:2** Mdo 15:4; 12; 1Kor 9:24; Flp 2:16
[g]**2:3** 2Kor 2:13; Mdo 16:3; 1Kor 9:21
[h]**2:4** 2Kor 11:26; Yud 24; Mdo 15:1; Gal 5:1, 13
[i]**2:5** Gal 2:14; 3:1; 4:16
[j]**2:6** Gal 6:3; Mdo 10:34
[k]**2:7** 1The 2:4; 1Tim 1:11; Mdo 9:15
[l]**2:8** Mdo 1:25; 1Kor 1:1; Mdo 9:15; 13:2; 22:21
[m]**2:9** 1Tim 3:15; Mdo 4:36; Rum 12:3; Mdo 15:13; Gal 2:7, 11, 14; 1Tim 3:15; Ufu 3:12
[n]9 Yaani Petro, pia mstari 11, 14.
[o]**2:10** Mdo 24:17; 11:30; 12:25; Rum 15:25; 1Kor 16:1; 2Kor 8:9
[p]**2:11** Mdo 11:19; 15:35
[q]**2:12** Mdo 11:2-3
[r]**2:13** Mdo 4:36
[s]**2:14** Mdo 10:28; 1Tim 5:20; Mdo 11:3
[t]**2:15** Flp 3:4-5; 1Sam 15:18

watu wa Mataifa, 16 [a]bado tunajua ya
kwamba mtu hahesabiwi haki kwa matendo
ya sheria bali kwa njia ya imani katika Yesu
Kristo. Hivyo sisi pia, tumemwamini Kristo
Yesu ili tupate kuhesabiwa haki kwa njia ya
imani katika Kristo, wala si kwa matendo
ya sheria, kwa sababu kwa kushika sheria
hakuna hata mtu mmoja atakayehesabiwa
haki.
17 [b]"Lakini tukitafuta kuhesabiwa haki
katika Kristo, inakuwa dhahiri kwamba sisi
ni wenye dhambi. Je, ina maana kwamba
Kristo amekuwa mtumishi wa dhambi?
La hasha! 18 Lakini ikiwa mimi ninajenga
tena kile ambacho nimekwisha kukibomoa,
basi ninaonyesha kwamba mimi ni mkosaji.
19 [c]Kwa maana mimi kwa njia ya sheria,
nimeifia sheria ili nipate kuishi kwa ajili ya
Mungu. 20 [d]Nimesulubiwa pamoja na Kristo,
wala si mimi tena ninayeishi, bali Kristo
ndiye aishiye ndani yangu. Uhai nilio nao
sasa katika mwili, ninaishi kwa imani ya
Mwana wa Mungu, aliyenipenda na kujitoa
kwa ajili yangu. 21 [e]Siibatilishi neema ya
Mungu, kwa maana kama haki ingeweza
kupatikana kwa njia ya sheria, basi Kristo
alikufa bure!"

*Imani Au Kushika Sheria?*

3 [f]Ninyi Wagalatia wajinga! Ni nani
aliyewaroga? Yesu Kristo aliwekwa
wazi mbele yenu kwamba amesulubiwa.
2 [g]Nataka nijifunze neno moja kutoka
kwenu: Je, mlipokea Roho wa Mungu
kwa kushika sheria, au kwa kuyaamini
yale mliyosikia? 3 [h]Je, ninyi ni wajinga
kiasi hicho? Baada ya kuanza kwa Roho,
je, sasa mwataka kumalizia katika mwili?
4 [i]Je, mlipata mateso kiasi hicho bure? Ni
kama kweli yalikuwa bure! 5 [j]Je, Mungu
huwapa Roho wake na kufanya miujiza
katikati yenu kwa sababu mnatii sheria,
au kwa sababu mnaamini kile mlichosikia?
6 [k]Kama vile "Abrahamu alimwamini
Mungu na ikahesabiwa kwake kuwa haki."
7 [l]Fahamuni basi kwamba wale walio na
imani, hao ndio watoto wa Abrahamu.
8 [m]Maandiko yakitabiri kwamba Mungu
angewahesabia haki watu wa Mataifa kwa
imani, alitangulia kumtangazia Abrahamu
Injili akisema kwamba, "Kwa kupitia kwako
mataifa yote yatabarikiwa." 9 [n]Kwa sababu
hii, wale wote wanaoamini wanabarikiwa
pamoja na Abrahamu, mtu wa imani.

*Sheria Na Laana*

10 [o]Kwa maana wote wanaotumainia
matendo ya sheria wako chini ya laana,
kwa kuwa imeandikwa, "Alaaniwe kila
mtu asiyeshikilia kutii mambo yote
yaliyoandikwa katika Kitabu cha Sheria."
11 [p]Basi ni dhahiri kwamba hakuna mtu
anayehesabiwa haki mbele za Mungu kwa
kushikilia sheria, kwa maana, "Mwenye
haki ataishi kwa imani." 12 [q]Lakini sheria
haitegemei imani. Kinyume chake, "Mtu
atendaye matendo hayo ataishi kwa hayo."
13 [r]Kristo alitukomboa kutoka laana ya
sheria kwa kufanyika laana kwa ajili yetu,
kwa maana imeandikwa, "Amelaaniwa yeye
aangikwaye juu ya mti." 14 [s]Alitukomboa ili
kwamba baraka aliyopewa Abrahamu ipate
kuwafikia watu wa Mataifa kwa njia ya
Kristo Yesu, ili kwa imani tupate kupokea
ile ahadi ya Roho.

[a]**2:16** Mdo 13:39; Rum 9:30
[b]**2:17** Gal 3:21
[c]**2:19** Rum 7:4; 6:10-14; 2Kor 5:15
[d]**2:20** Rum 6:6; 1Pet 4:2; Mt 4:3; Rum 8:37; Gal 1:4
[e]**2:21** Gal 3:21
[f]**3:1** Gal 5:7; 1Kor 1:23
[g]**3:2** Rum 10:17; Yn 20:22; Gal 3:5, 10; 2:16; Rum 10:17
[h]**3:3** Gal 4:9; Ebr 7:16; 9:10
[i]**3:4** Ebr 10:35, 36; 2Yn 8
[j]**3:5** 1Kor 12:10; 2Kor 3:8
[k]**3:6** Mwa 15:6; Rum 4:3
[l]**3:7** Yn 8:39; Rum 4:11, 12, 16
[m]**3:8** Mwa 18:18; Mdo 3:25
[n]**3:9** Rum 4:16; Gal 3:7; Rum 4:18-22
[o]**3:10** Kum 27:26; Yer 11:3
[p]**3:11** Gal 2:16; Hab 2:4; Rum 1:17; Ebr 10:38
[q]**3:12** Rum 4:4, 5; Law 18:5; Neh 9:29; Eze 20:11
[r]**3:13** Rum 8:3; 2Kor 5:21; 4:5; Kum 21:23
[s]**3:14** Rum 4:9, 16; Isa 32:15; 44:3; Yer 31:33; 32:40; Eze 11:19

*Sheria Na Ahadi*

[15] [a]Ndugu zangu, nataka nitoe mfano
kutoka maisha ya kila siku. Kama vile
hakuna mtu awezaye kutangua au kuongeza
kitu katika agano la mtu ambalo limekwisha
kuthibitishwa, vivyo hivyo kwa hali kama
hii. [16] [b]Ahadi zilinenwa kwa Abrahamu na
kwa mzao wake. Maandiko hayasemi "kwa
wazao," likimaanisha watu wengi, bali
"kwa mzao wako," yaani mtu mmoja, ndiye
Kristo. [17] [c]Ninachotaka kusema ni kwamba,
sheria, ambayo ilitolewa miaka 430
baadaye, haitangui Agano lililothibitishwa
na Mungu ili kuibatilisha ahadi ile. [18] [d]Kwa
maana kama urithi hupatikana kwa sheria,
basi hautegemei tena ahadi, lakini Mungu
kwa neema yake alimpa Abrahamu urithi
kwa njia ya ahadi.

*Kusudi La Sheria*

[19] [e]Kwa nini basi iwepo sheria? Sheria
iliwekwa kwa sababu ya makosa mpaka
atakapokuja yule Mzao wa Abrahamu,
ambaye alitajwa katika ile ahadi. Sheria
iliamriwa na malaika kwa mkono wa
mpatanishi. [20] [f]Basi mpatanishi huhusisha
zaidi ya upande mmoja, lakini Mungu ni
mmoja.

[21] [g]Je basi, sheria inapingana na ahadi
za Mungu? La hasha! Kwa maana kama
sheria iliyotolewa ingeweza kuwapa watu
uzima, basi haki ingepatikana kwa njia ya
sheria. [22] [h]Lakini Maandiko yamefanya vitu
vyote vifungwe chini ya nguvu ya dhambi,
ili yale yaliyoahidiwa kwa njia ya imani
katika Yesu Kristo yapate kupewa wale
wanaoamini.

[23] [i]Kabla imani hii haijaja tulikuwa
tumewekwa chini ya sheria, tumefungwa
mpaka ile imani ifunuliwe. [24] [j]Hivyo, sheria
ilikuwa kiongozi kutufikisha kwa Kristo,
ili tupate kuhesabiwa haki kwa imani.
[25] [k]Lakini sasa kwa kuwa ile imani imekuja,
hatusimamiwi tena na sheria.

*Watoto Wa Mungu*

[26] [l]Kwa maana ninyi nyote mmekuwa
watoto wa Mungu katika Kristo Yesu
kwa njia ya imani. [27] [m]Kwa maana wote
mliobatizwa ndani ya Kristo, mmemvaa
Kristo. [28] [n]Wala hakuna tena Myahudi au
Myunani, mtumwa au mtu huru, mwanaume
wala mwanamke, maana nyote mmekuwa
wamoja ndani ya Kristo Yesu. [29] [o]Nanyi
mkiwa ni mali ya Kristo, basi ninyi ni wa
uzao wa Abrahamu na warithi sawasawa
na ile ahadi.

4 Lile nisemalo ni kwamba wakati wote
mrithi bado ni mtoto, hana tofauti na
mtumwa, ingawa ndiye mmiliki wa mali
yote. [2] Yeye huwa yuko chini ya uangalizi
wa walezi na wadhamini mpaka ufike
wakati uliowekwa na baba yake. [3] [p]Vivyo
hivyo na sisi, tulipokuwa bado watoto
wadogo, tulikuwa utumwani chini ya
taratibu za kawaida za ulimwengu. [4] [q]Lakini
ulipowadia utimilifu wa wakati, Mungu
alimtuma Mwanawe, ambaye alizaliwa
na mwanamke, akazaliwa chini ya sheria,
[5] [r]kusudi awakomboe wale waliokuwa
chini ya sheria, ili tupate kupokea zile
haki kamili za kufanywa watoto wa Mungu.
[6] [s]Kwa sababu ninyi ni watoto wa Mungu,
Mungu amemtuma Roho wa Mwanawe

---

[a]**3:15** Ebr 9:17; Rum 7:1
[b]**3:16** Mwa 17:19; Za 132:11; Mik 7:20; Lk 1:55; Rum 4:13, 16
[c]**3:17** Mwa 15:13, 14; Kut 12:40; Mdo 7:6
[d]**3:18** Rum 4:14
[e]**3:19** Rum 5:20; 3:16; Kum 33:2; Mdo 7:53; Kut 20:19
[f]**3:20** 1Tim 2:5; Ebr 8:6; 9:15; 12:24
[g]**3:21** Gal 2:17; Rum 7:12; Gal 2:21
[h]**3:22** Rum 3:9-19; 11:32
[i]**3:23** Rum 11:32; Gal 3:25
[j]**3:24** Gal 3:19; Rum 10:4; 4:15; Gal 2:16
[k]**3:25** Rum 7:4; 10:4
[l]**3:26** Rum 8:14; Yn 1:12; Rum 8:15, 16; Gal 4:5; 1Yn 3:1
[m]**3:27** Rum 6:3; 13:14; Mt 28:19
[n]**3:28** 1Kor 12:13; Kol 3:11; Mwa 1:27; 5:2; Yoe 2:29; Yn 10:16
[o]**3:29** 1Kor 3:22; Gal 3:16; Lk 3:8; Rum 8:17; Gal 3:16
[p]**4:3** Gal 4:9; 5:1; Kol 2:8, 20; Ebr 9:10
[q]**4:4** Mk 1:15; Rum 5:6; Efe 1:10; Yn 3:17; 1:14; Lk 2:27
[r]**4:5** Rum 3:24; Yn 1:12; Rum 8:14
[s]**4:6** Mdo 16:7; Rum 5:5; 8:15, 16

mioyoni mwetu, anayelia, “Abba,[a] Baba.”
7 [b]Kwa hiyo, wewe si mtumwa tena, bali ni
mtoto, kwa kuwa wewe ni mtoto, Mungu
amekufanya wewe pia kuwa mrithi kwa
kupitia Kristo.

*Paulo Awashawishi Wagalatia*

8 [c]Zamani, mlipokuwa hammjui Mungu,
mlikuwa watumwa wa viumbe ambavyo
kwa asili si Mungu. 9 [d]Lakini sasa kwa kuwa
mmemjua Mungu, au zaidi mmejulikana na
Mungu, inakuwaje mnarejea tena katika
zile kanuni za kwanza zenye udhaifu
na upungufu? Mnataka ziwafanye tena
watumwa? 10 [e]Mnaadhimisha siku maalum,
miezi, nyakati na miaka! 11 [f]Nina hofu juu
yenu, kwamba kazi niliyofanya kwa ajili
yenu inaweza kuwa nimejitaabisha bure.

12 [g]Ndugu zangu, nawasihi mwe kama
mimi, kwa sababu mimi nimekuwa kama
ninyi. Hamkunitendea jambo lolote baya.
13 [h]Ninyi mwajua kwamba ni kwa ajili
ya udhaifu wangu niliwahubiria Injili.
14 [i]Ingawa hali yangu iliwatia majaribuni,
hamkunidharau wala kunidhihaki, bali
mlinikaribisha kama malaika wa Mungu,
kama vile Kristo Yesu. 15 Ile hali ya furaha
mliyokuwa nayo imekwenda wapi? Naweza
kushuhudia kwamba, kama ingewezekana
mngeng’oa macho yenu na kunipa mimi.
16 [j]Je, sasa nimekuwa adui yenu kwa
kuwaambia kweli?

17 [k]Hao wana shauku ya kuwapata
lakini si kwa kusudi zuri. Wanachotaka
ni kuwatenga mbali nasi, ili ninyi mpate
kuwaonea wao shauku. 18 [l]Ni vizuri wakati
wote kuwa na shauku kwa ajili ya kusudi
zuri, si wakati nikiwa pamoja nanyi tu.
19 [m]Watoto wangu wapendwa, ambao
kwa mara nyingine ninawaonea utungu,
ninatamani kwamba Kristo aumbike ndani
yenu. 20 Natamani kama ningekuwa pamoja
nanyi sasa, pengine ningebadilisha sauti
yangu. Kwa maana nina wasiwasi kwa ajili
yenu.

*Mfano Wa Hagari Na Sara*

21 [n]Niambieni, ninyi mnaotaka kuwa chini
ya sheria, je, hamjui sheria inavyosema?
22 Kwa maana imeandikwa kwamba
Abrahamu alikuwa na wana wawili,
mmoja wa mwanamke mtumwa na wa
pili wa mwanamke huru. 23 [o]Lakini, mtoto
wa mwanamke mtumwa alizaliwa kwa
mapenzi ya mwili, na yule mwingine wa
mwanamke huru alizaliwa kutokana na
ahadi ya Mungu.

24 Mambo haya yanaweza kuchukuliwa
kama mfano. Kwa maana hao wanawake
wawili ni mfano wa maagano mawili:
Agano la kwanza, ni lile lililofanyika
katika Mlima Sinai, lizaalo watoto wa
utumwa. Hili ndilo huyo Hagari. 25 Basi
Hagari anawakilisha Mlima Sinai ulioko
Arabuni, na unafanana na Yerusalemu
ya sasa ambayo iko utumwani pamoja na
watoto wake. 26 [p]Lakini Yerusalemu wa juu
ni huru, nayo ndiye mama yetu. 27 [q]Kwa
maana imeandikwa:

“Furahi, ewe mwanamke tasa,
 wewe usiyezaa;
paza sauti, na kuimba kwa furaha,
 wewe usiyepatwa na utungu wa
  kuzaa;

[a]6 Abba ni neno la Kiaramu ambalo maana yake ni Baba; lingeweza kutumiwa tu na mtoto wa kuzaa.
[b]**4:7** Rum 8:17; Gal 3:29
[c]**4:8** Rum 1:28; 1Kor 1:21; 15:34; 1The 4:5; 2The 1:8; Gal 4:3
[d]**4:9** 1Kor 8:3; Gal 4:3; Kol 2:20
[e]**4:10** Rum 14:5; Kol 2:16
[f]**4:11** 1The 3:5; Gal 2:2; 5:2, 4
[g]**4:12** Rum 7:1; Gal 6:18; 2Kor 2:5
[h]**4:13** 1Kor 2:3; 2Kor 11:30; 12:7, 9; Gal 1:6
[i]**4:14** Mt 10:40; 2Sam 19:27; Mal 2:7; Zek 12:8; Mt 10:40; Lk 10:16
[j]**4:16** Gal 2:5, 14; Amo 5:10
[k]**4:17** Gal 2:4, 12; Rum 10:12; 1Kor 11:2
[l]**4:18** Gal 4:13, 14
[m]**4:19** 1The 2:11; Rum 8:29; Efe 4:13
[n]**4:21** Rum 2:12
[o]**4:23** Gal 4:28, 29; Rum 9:7, 8; Mwa 17:16-21; 18:10-14; 4:24
[p]**4:26** Flp 2:3; Ebr 12:22; Isa 2:2; Ufu 3:12; 21:2, 10
[q]**4:27** Isa 54:1

kwa maana watoto wa mwanamke
aliyeachwa ukiwa ni wengi
kuliko wa mwanamke mwenye
mume.”

28 [a]Basi, sisi ndugu zangu, ni kama Isaki,
tu watoto wa ahadi. 29 [b]Lakini, kama vile
ilivyokuwa siku zile yule aliyezaliwa kwa
mwili alivyomchokoza yule aliyezaliwa kwa
Roho, ndivyo ilivyo hata sasa. 30 [c]Lakini
Maandiko yasemaje? “Mwondoe mwanamke
mtumwa pamoja na mwanawe, kwa sababu
mwana wa mwanamke mtumwa kamwe
hatarithi pamoja na mwana wa aliye huru.”
31 [d]Kwa hiyo ndugu zangu, sisi si watoto wa
mwanamke mtumwa, bali wa yule aliye
huru.

### *Uhuru Ndani Ya Kristo*

5 [e]Kristo alitupa uhuru, akataka tubaki
huru. Hivyo simameni imara wala
msikubali tena kulemewa na kongwa la
utumwa.
2 [f]Sikilizeni! Mimi, Paulo, nawaambieni
kwamba kama mkikubali kutahiriwa,
basi Kristo hatawafaidia chochote.
3 [g]Namshuhudia tena kila mtu anayekubali
kutahiriwa kwamba inampasa kushika
sheria yote. 4 [h]Ninyi mnaotafuta kuhesabiwa
haki kwa njia ya sheria mmetengwa na
Kristo, mko mbali na neema ya Mungu.
5 [i]Kwa maana, kwa njia ya Roho kwa
imani, tunangojea kwa shauku tumaini la
haki. 6 [j]Kwa maana ndani ya Kristo Yesu,
kutahiriwa au kutokutahiriwa hakuleti
tofauti, bali lililo muhimu ni imani itendayo
kazi kwa njia ya upendo.
7 [k]Mlikuwa mkipiga mbio vizuri. Ni nani
aliyewazuia msiitii kweli? 8 [l]Ushawishi
wa namna hiyo haukutokana na yule
anayewaita. 9 [m]“Chachu kidogo huchachua
donge zima.” 10 [n]Nina hakika katika
Bwana kwamba hamtakuwa na msimamo
mwingine. Mtu anayewachanganya
anastahili adhabu, hata awe nani.
11 [o]Lakini ndugu zangu, kama mimi bado
ninahubiri kuhusu kutahiriwa, kwa nini
bado ninateswa? Katika hiyo hali basi,
kwazo la msalaba limeondolewa. 12 [p]Laiti
hao wanaowavuruga wangejihasi wao
wenyewe!
13 [q]Ndugu zangu, ninyi mliitwa ili mwe
huru, hivyo msitumie uhuru wenu kama
fursa ya kufuata tamaa za mwili, bali
tumikianeni ninyi kwa ninyi kwa upendo.
14 [r]Kwa maana sheria yote hukamilika katika
amri moja: “Mpende jirani yako kama nafsi
yako.” 15 Kama mkiumana na kutafunana,
angalieni, msije mkaangamizana.

### *Maisha Ya Kiroho*

16 [s]Kwa hiyo nasema, enendeni kwa
Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa
za mwili. 17 [t]Kwa maana mwili hutamani
yale yaliyo kinyume na Roho, naye Roho
hutamani yale yaliyo kinyume na mwili.
Roho na mwili hupingana na kwa sababu
hiyo hamwezi kufanya mnayotaka. 18 [u]Lakini
kama mkiongozwa na Roho, hamko chini
ya sheria.
19 [v]Basi matendo ya mwili ni dhahiri
nayo ni haya: Uasherati, uchafu, ufisadi,
20 kuabudu sanamu, uchawi, uadui,
ugomvi, wivu, hasira, fitina, faraka, uzushi,

---

[a]**4:28** Mdo 3:25; Rum 9:8; Gal 3:29
[b]**4:29** Mwa 21:9; Gal 5:11; 6:12
[c]**4:30** Mwa 21:10
[d]**4:31** Rum 7:4; Gal 4:22
[e]**5:1** Gal 5:13; 2:4; Yn 8:32; Rum 7:4; 1Kor 16:13; Mt 23:4
[f]**5:2** Gal 5:3; Mdo 15:1
[g]**5:3** Rum 2:25; Gal 3:10; Yak 2:10
[h]**5:4** Rum 3:28; Ebr 12:15; 2Pet 3:17
[i]**5:5** Rum 8:23, 24; 2Tim 4:8; 1Kor 7:19
[j]**5:6** Rum 16:3; 1Kor 7:19; 1The 1:3; Yak 2:22
[k]**5:7** 1Kor 9:24; Gal 3:1
[l]**5:8** Rum 8:28; Gal 1:6
[m]**5:9** 1Kor 5:6; 15:33
[n]**5:10** 2Kor 2:3; Flp 3:15; Gal 1:7
[o]**5:11** Gal 4:29; 6:12; Lk 2:34
[p]**5:12** Gal 5:10; Yos 7:25; 1Kor 5:13; Gal 1:8, 9; Mdo 15:1, 2, 24
[q]**5:13** Gal 5:1, 24; 1Kor 8:9; 1Pet 2:16; 1Kor 9:19; 2Kor 4:5
[r]**5:14** Law 19:18; Mt 5:43; Gal 6:2
[s]**5:16** Gal 5:18, 25; Rum 8:2, 4-6, 9; 14; 2Kor 5:17; Gal 5:14
[t]**5:17** Rum 8:5-8; 7:15-23
[u]**5:18** Rum 2:12; 6:14; Gal 5:16; 1Tim 1:9
[v]**5:19** 1Kor 6:18; 3:3; Efe 5:3; Kol 3:5; Yak 3:14, 15

21 [a]husuda, ulevi, ulafi na mambo mengine
yanayofanana na hayo. Nawaonya, kama
nilivyokwisha kuwaonya kabla, kwamba
watu watendao mambo kama hayo,
hawatataurithi Ufalme wa Mungu.
22 [b]Lakini tunda la Roho ni upendo,
furaha, amani, uvumilivu, utu wema,
fadhili, uaminifu, 23 upole na kiasi. Katika
mambo kama haya hakuna sheria. 24 Wote
walio wa Kristo Yesu wameusulubisha
mwili na shauku zake pamoja na tamaa
zake. 25 Kwa kuwa tunaishi kwa Roho, basi,
tuenende kwa Roho. 26 [c]Tusijisifu bure,
tukichokozana na kuoneana wivu.

*Chukulianeni Mizigo*

6 [d]Ndugu zangu, ikiwa mtu ameghafilika
akatenda dhambi, basi ninyi mlio
wa rohoni, mrejesheni upya mtu huyo
kwa roho ya upole. Lakini jihadharini,
ili ninyi wenyewe msije mkajaribiwa.
2 [e]Chukulianeni mizigo ninyi kwa ninyi,
nanyi kwa njia hii mtatimiza sheria ya
Kristo. 3 [f]Kama mtu yeyote akijiona kuwa
yeye ni bora na kumbe sivyo, basi mtu
huyo anajidanganya mwenyewe. 4 [g]Lakini
kila mtu na aipime kazi yake mwenyewe,
ndipo aweze kujisifu, bila kujilinganisha
na mtu mwingine. 5 [h]Kwa maana, kila
mtu atauchukua mzigo wake mwenyewe.
6 [i]Basi, yeye afundishwaye katika neno na
amshirikishe mwalimu wake mema yote.
7 [j]Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi.
Kwa kuwa kile apandacho mtu ndicho
atakachovuna. 8 [k]Apandaye kwa mwili,
katika mwili wake atavuna uharibifu,
lakini yeye apandaye katika Roho, katika
Roho atavuna uzima wa milele. 9 [l]Hivyo,
tusichoke katika kutenda mema, kwa kuwa
tutavuna kwa wakati wake tusipokata
tamaa. 10 Kwa hiyo, kadiri tupatavyo nafasi
na tuwatendee watu wote mema, hasa wale
wa jamaa ya waaminio.

*Si Kutahiriwa Bali Kuwa Kiumbe Kipya*

11 Angalieni herufi kubwa nitumiazo
ninapowaandikia kwa mkono wangu
mwenyewe!
12 Wale wanaotaka kuonekana wazuri kwa
mambo ya mwili wanataka wawalazimishe
kutahiriwa. Sababu pekee ya kufanya hivyo
ni kuepuka kuteswa kwa ajili ya msalaba
wa Kristo. 13 Hata wale waliotahiriwa
wenyewe hawaitii sheria, lakini wanataka
ninyi mtahiriwe ili wapate kujivuna kwa
habari ya miili yenu. 14 Mungu apishie
mbali nisije nikajivunia kitu chochote
isipokuwa msalaba wa Bwana wetu Yesu
Kristo, ambaye kwa yeye ulimwengu
umesulubiwa kwangu, nami nimesulubiwa
kwa ulimwengu. 15 Kwa maana katika Kristo
Yesu, kutahiriwa au kutokutahiriwa si
kitu, bali kule kuwa kiumbe kipya ni kila
kitu! 16 Amani na rehema viwe na wote
wanaofuata kanuni hii, na juu ya Israeli
wa Mungu.
17 Hatimaye, tangu sasa mtu yeyote
asinitaabishe, kwa maana nachukua katika
mwili wangu chapa zake Yesu.
18 Ndugu zangu, neema ya Bwana wetu
Yesu Kristo iwe pamoja na roho zenu.
Amen.

---

[a]**5:21** Rum 13:13; Mt 15:19; 25:34; 1Kor 6:9
[b]**5:22** Mt 7:16-20
[c]**5:26** Flp 2:3; Mt 18:15; Yak 2:19
[d]**6:1** 1Kor 2:15; Rum 14:1; 15:1; Ebr 12:13; Yak 5:19; 1Kor 2:15; 3:1; 4:21; 2The 3:15; 1Kor 7:5
[e]**6:2** Rum 15:1; 1Kor 9:21; Rum 15:1; Gal 5:13; 1The 5:14; Yn 13:14, 15, 34; 15:12; Yak 2:8
[f]**6:3** Rum 12:3; 1Kor 8:2; Rum 12:3; 1Kor 8:2; Gal 2:6; 2Kor 3:5; 12:11
[g]**6:4** 1Kor 11:28; 2Kor 13:5; Lk 18:11
[h]**6:5** Rum 2:6; 1Kor 3:8
[i]**6:6** 1Kor 9:11, 14; Rum 15:27; 1Kor 9:11, 14
[j]**6:7** 1Kor 6:9; 2Kor 9:6; 1Kor 15:33; Ay 13:9; Lk 16:25; Rum 2:6
[k]**6:8** Hos 8:7; Rum 6:23; Yn 3:18; Ay 4:8; Mit 11:18; 22:8; Hos 8:7; 10:12; Rum 8:13; Yak 3:18
[l]**6:9** 1Kor 15:58; Za 126:5; 2Kor 4:1; Ay 42:12; Ebr 12:3; Ufu 2:10

# WAEFESO

*Salamu*

1 [a]Paulo, mtume wa Kristo Yesu, kwa
mapenzi ya Mungu:
Kwa watakatifu walioko Efeso, walio
waaminifu katika Kristo Yesu:
2 [b]Neema na amani itokayo kwa Mungu
Baba yetu na kwa Bwana wetu Yesu Kristo
iwe nanyi.

*Baraka Za Kiroho Katika Kristo Yesu*

3 [c]Ahimidiwe Mungu na Baba wa
Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki
sisi kwa baraka zote za rohoni, katika
ulimwengu wa roho ndani ya Kristo. 4 [d]Kwa
maana alituchagua katika yeye kabla ya
kuumbwa ulimwengu ili tuwe watakatifu
na bila lawama mbele zake. Kwa upendo
5 [e]alitangulia kutuchagua tuwe wanawe
kwa njia ya Yesu Kristo kwa furaha yake
na mapenzi yake mwenyewe. 6 [f]Kwa hiyo
tunamsifu Mungu kwa huruma zake kuu
alizotumiminia sisi katika Mwanawe
Mpendwa. 7 [g]Ndani yake tunao ukombozi
kwa njia ya damu yake, yaani, msamaha wa
dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake
8 [h]aliyotumiminia kwa wingi, kwa hekima
yote na maarifa yote. 9 [i]Naye alitujulisha
siri ya mapenzi yake sawasawa na uradhi
wa mapenzi yake, ambayo alikusudia katika
Kristo, 10 [j]ili yapate kutimizwa wakati
mkamilifu utakapowadia, yaani, kuvitia
vitu vyote vya mbinguni na vya duniani
pamoja, chini ya kiongozi mmoja, ndiye
Kristo.
11 [k]Katika Kristo sisi nasi tumepata urithi,
tukisha kuchaguliwa sawasawa na kusudi la
Mungu, yeye ambaye hufanya mambo yote
kulingana na kusudi la mapenzi yake, 12 [l]ili
kwamba, sisi tuliokuwa wa kwanza kuweka
tumaini katika Kristo, tupate kuishi kwa
sifa ya utukufu wake. 13 [m]Ninyi pia mliingia
ndani ya Kristo mliposikia Neno la kweli,
Injili ya wokovu wenu. Mkiisha kuamini,
ndani yake mlitiwa muhuri, yaani, Roho
Mtakatifu mliyeahidiwa, 14 [n]yeye ambaye
ni amana yetu akituhakikishia urithi wetu
hadi ukombozi wa wale walio milki ya
Mungu kwa sifa ya utukufu wake.

*Shukrani Na Maombi*

15 [o]Kwa sababu hii, tangu niliposikia
juu ya imani yenu katika Bwana Yesu
na upendo wenu kwa watakatifu wote,
16 [p]sijaacha kumshukuru Mungu kwa ajili
yenu, nikiwakumbuka katika maombi
yangu. 17 [q]Nazidi kumwomba Mungu
wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa
utukufu, awajalieni ninyi roho ya hekima
na ya ufunuo, ili mpate kumjua zaidi.
18 [r]Ninaomba pia kwamba macho ya mioyo
yenu yatiwe nuru ili mpate kujua tumaini
mliloitiwa, utajiri wa urithi wa utukufu
wake kwa watakatifu 19 [s]na uweza wake
mkuu usiolinganishwa kwa ajili yetu sisi
tuaminio. Uweza huo unaofanya kazi
ndani yetu, ni sawa na ile nguvu kuu mno
20 [t]aliyoitumia katika Kristo alipomfufua
kutoka kwa wafu, na akamketisha mkono
wake wa kuume huko mbinguni, 21 [u]juu
sana kuliko falme zote na mamlaka, enzi na

[a]**1:1** 1Kor 1:1; 2Kor 1:1; Kol 1:2
[b]**1:2** Rum 1:7; Kol 1:2; Gal 1:3; Tit 1:4
[c]**1:3** 2Kor 2:1, 3; Efe 3:10; 6:12
[d]**1:4** Za 15:2; Kol 1:22; Efe 4:2, 15, 16
[e]**1:5** Rum 8:29, 30; Lk 12:32; 1Kor 1:21
[f]**1:6** Mt 3:17; Efe 1:12, 14; Kol 1:13
[g]**1:7** Rum 3:24; Kol 1:14, 20; Efe 2:7; 3:8, 16; Mdo 20:28; Ebr 9:14; 1Pet 1:16
[h]**1:8** Kol 1:9
[i]**1:9** Rum 16:25; Efe 2:7; 3:9
[j]**1:10** Mk 1:15; Kol 1:20
[k]**1:11** Rum 8:28
[l]**1:12** Efe 1:6, 14; 2The 2:13; Yak 1:18
[m]**1:13** Efe 4:21; 4:30; Yn 1:17; 2Kor 6:7
[n]**1:14** Mdo 20:32; 1Kor 1:22; 5:5
[o]**1:15** Kol 1:4; Flm 5
[p]**1:16** Rum 1:8; Flp 1:3, 4; Kol 1:3; 1The 1:2; 2The 1:3
[q]**1:17** Rum 15:6; Kut 28:3
[r]**1:18** Ay 42:5; Ebr 6:4
[s]**1:19** Kol 1:29; Efe 6:10
[t]**1:20** Mdo 2:24; Za 110:1; Mdo 7:55, 56; Kol 3:1; Ebr 1:3; 10:12
[u]**1:21** Flp 2:9, 10; Kol 2:10; Ebr 1:4; Rum 8:38

milki, na juu ya kila jina litajwalo, si katika
ulimwengu huu tu, bali katika ule ujao
pia. 22 [a]Naye Mungu ameweka vitu vyote
viwe chini ya miguu yake na amemfanya
yeye awe kichwa cha vitu vyote kwa ajili
ya Kanisa, 23 ambalo ndilo mwili wake,
ukamilifu wake yeye aliye yote katika yote.

### *Tumefanywa Kuwa Hai Ndani Ya Kristo*

2 [b]Kwa habari zenu, mlikuwa wafu katika
makosa na dhambi zenu, 2 [c]ambazo
mlizitenda mlipofuatisha namna ya
ulimwengu huu na za yule mtawala wa
ufalme wa anga, yule roho atendaye kazi
sasa ndani ya wale wasiotii. 3 [d]Sisi sote pia
tuliishi katikati yao hapo zamani, tukitimiza
tamaa za asili yetu ya dhambi na kufuata
tamaa zake na mawazo yake. Nasi kwa asili
tulikuwa wana wa ghadhabu, kama mtu
mwingine yeyote. 4 [e]Lakini Mungu kwa
upendo wake mwingi kwetu sisi, ambaye ni
mwingi wa rehema, 5 [f]hata tulipokuwa wafu
kwa ajili ya makosa yetu, alitufanya tuwe hai
pamoja na Kristo Yesu, yaani, mmeokolewa
kwa neema. 6 [g]Mungu alitufufua pamoja
na Kristo na kutuketisha pamoja naye
katika ulimwengu wa roho katika Kristo
Yesu, 7 [h]ili katika ule ulimwengu ujao
apate kuonyesha wingi wa neema yake
isiyopimika, iliyodhihirishwa kwetu kwa
wema wake ndani ya Kristo Yesu. 8 [i]Kwa
maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia
ya imani, wala si kwa matendo yenu mema.
Hii ni zawadi kutoka kwa Mungu, 9 [j]si kwa
matendo, ili mtu yeyote asije akajisifu.
10 [k]Kwa maana sisi ni kazi ya mikono ya
Mungu, tulioumbwa katika Kristo Yesu, ili
tupate kutenda matendo mema, ambayo
Mungu alitangulia kuyaandaa tupate kuishi
katika hayo.

### *Wamoja Katika Kristo*

11 [l]Kwa hiyo kumbukeni kwamba ninyi
ambao hapo awali mlikuwa watu wa Mataifa
kwa kuzaliwa na kuitwa "wasiotahiriwa"
na wale wanaojiita "waliotahiriwa" (yaani
tohara ifanyikayo katika mwili kwa mikono
ya wanadamu), 12 [m]kumbukeni kwamba
wakati ule mlikuwa mbali na Kristo, mkiwa
mmetengwa kutoka jumuiya ya Israeli, na
mkiwa wageni katika yale maagano ya
ahadi, nanyi mkiwa hamna tumaini wala
Mungu duniani. 13 [n]Lakini sasa katika Kristo
Yesu, ninyi ambao hapo kwanza mlikuwa
mbali na Mungu, sasa mmeletwa karibu
kwa njia ya damu ya Kristo.

14 [o]Kwa maana yeye mwenyewe ndiye
amani yetu, aliyetufanya sisi tuliokuwa
wawili, yaani, Wayahudi na watu wa
Mataifa, tuwe wamoja kwa kuvunja kizuizi
na kubomoa ule ukuta wa uadui uliokuwa
kati yetu, 15 [p]kwa kuibatilisha ile sheria
pamoja na amri zake na maagizo yake
alipoutoa mwili wake, ili apate kufanya
ndani yake mtu mmoja mpya badala ya
hao wawili, hivyo akifanya amani, 16 [q]naye
katika mwili huu mmoja awapatanishe
wote wawili na Mungu kupitia msalaba, ili
kwa huo msalaba akaangamiza uadui wao.
17 [r]Alikuja na kuhubiri amani kwenu ninyi
mliokuwa mbali na pia akahubiri amani
kwao waliokuwa karibu. 18 [s]Kwa maana
kwa kupitia kwake, sisi sote tunaweza
kumkaribia Baba katika Roho mmoja.

19 [t]Hivyo basi, ninyi sasa si wageni tena
wala wapitaji, bali mmekuwa wenyeji
pamoja na watakatifu na pia jamaa wa

---

[a]**1:22** Mt 28:18; 1Kor 11:3; Kol 2:19
[b]**2:1** Kol 2:13; Yn 5:24; Kol 2:13; Efe 2:5; 4:18
[c]**2:2** Tit 3:3; Yn 12:31; Efe 5:6
[d]**2:3** Gal 5:16-24; Kol 3:6; Tit 3:3; 1Pet 4:3; Gal 5:16; Za 51:5; Rum 5:12, 14
[e]**2:4** Yn 3:16; Rum 10:12; Efe 1:7; 2:7
[f]**2:5** Efe 2:1; 2:8; Za 103:12; Yn 5:24; Mdo 15:11
[g]**2:6** Efe 1:3, 20; Rum 8:10; Flp 3:20
[h]**2:7** Tit 3:4; Efe 1:7; Rum 2:4
[i]**2:8** Rum 4:2; 2Tim 1:9; Tit 3:5
[j]**2:9** Kum 9:5; 1Kor 1:29
[k]**2:10** Efe 4:24; Tit 2:14; Isa 29:23; 43:7; 60:21; Tit 2:14
[l]**2:11** Kol 2:11; Efe 5:8; 2:2
[m]**2:12** Gal 3:17; 1The 4:13
[n]**2:13** Mdo 2:39; Kol 1:20
[o]**2:14** 1Kor 12:13; Isa 9:5; Gal 3:28; Kol 2:14
[p]**2:15** Kol 1:21-22; 2:14; Gal 3:28
[q]**2:16** Kol 1:20, 22; Rum 6:6; 8:3; Kol 2:14
[r]**2:17** Za 148:14; Isa 57:19
[s]**2:18** Efe 3:12; Kol 1:12; 1Kor 12:13
[t]**2:19** Flp 3:20; Gal 6:10

nyumbani mwake Mungu. 20 [a]Mmejengwa
juu ya msingi wa mitume na manabii,
naye Kristo Yesu mwenyewe ndiye jiwe
kuu la pembeni. 21 [b]Ndani yake jengo
lote limeshikamanishwa pamoja na
kusimamishwa ili kuwa Hekalu takatifu
katika Bwana. 22 Katika yeye ninyi nanyi
mnajengwa pamoja ili mpate kuwa makao
ambayo Mungu anaishi ndani yake kwa njia
ya Roho wake.

*Huduma Ya Paulo Kwa Watu Wa Mataifa*

3 [c]Kwa sababu hii, mimi Paulo, mfungwa
wa Kristo Yesu kwa ajili yenu ninyi watu
wa Mataifa:

2 [d]Kwa hakika mmekwisha kusikia
kuhusu ile huduma ya neema ya Mungu
niliyopewa kwa ajili yenu, 3 [e]yaani, ile
siri iliodhihirishwa kwangu kwa njia ya
ufunuo, kama nilivyotangulia kuandika
kwa kifupi. 4 [f]Kwa kusoma haya, basi
mtaweza kuelewa ufahamu wangu katika
siri ya Kristo. 5 [g]Siri hii haikudhihirishwa
kwa wanadamu katika vizazi vingine kama
vile sasa ilivyodhihirishwa na Roho kwa
mitume na manabii watakatifu wa Mungu.
6 [h]Siri hii ni kwamba, kwa njia ya Injili, watu
wa Mataifa ni warithi pamoja na Israeli,
viungo vya mwili mmoja na washiriki
pamoja wa ahadi katika Kristo Yesu.

7 [i]Nimekuwa mtumishi wa Injili hii kwa
kipawa cha neema ya Mungu niliyopewa
kwa nguvu yake itendayo kazi. 8 [j]Ingawa
mimi ni mdogo kuliko aliye mdogo kabisa
miongoni mwa watakatifu wote, nilipewa
neema hii: ili niwahubirie watu wa Mataifa
kuhusu utajiri usiopimika ulio ndani ya
Kristo, 9 [k]na kuweka wazi kwa kila mtu
siri hii iliyokuwa imefichwa tangu zamani
katika Mungu, aliyeumba vitu vyote. 10 [l]Ili
sasa kwa njia ya Kanisa, hekima yote ya
Mungu ipate kujulikana kwa watawala
na wenye mamlaka katika ulimwengu wa
roho, 11 [m]sawasawa na kusudi lake la milele
katika Kristo Yesu Bwana wetu. 12 [n]Ndani
yake na kwa njia ya imani katika yeye
twaweza kumkaribia Mungu kwa uhuru
na kwa ujasiri. 13 [o]Kwa hiyo, nawaomba
msikate tamaa kwa sababu ya mateso yangu
kwa ajili yenu, hayo ni utukufu wenu.

*Maombi Ya Paulo Kwa Waefeso*

14 [p]Kwa sababu hii nampigia Baba magoti,
15 [q]ambaye ubaba wote wa kila jamaa za
mbinguni na za duniani unatokana naye.
16 [r]Namwomba Mungu awaimarishe kwa
kuwatia nguvu mioyo yenu kwa njia ya
Roho wake kwa kadiri ya utajiri wa utukufu
wake, 17 [s]ili kwamba, Kristo apate kukaa
mioyoni mwenu kwa njia ya imani. Nami
ninaomba kwamba ninyi mkiwa wenye
mizizi tena imara katika msingi wa upendo,
18 mwe na uwezo wa kufahamu pamoja na
watakatifu wote jinsi ulivyo upana, urefu,
kimo na kina upendo wa Kristo, 19 [t]na kujua
upendo huu unaopita fahamu, ili mpate
kujazwa na kufikia kipimo cha ukamilifu
wote wa Mungu.

20 [u]Basi kwa yeye awezaye kutenda
mambo ya ajabu yasiyopimika kuliko yote
tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya
uweza wake ule utendao kazi ndani yetu,
21 [v]yeye atukuzwe katika kanisa na katika

---

[a]**2:20** Mt 16:18; 1Kor 3:10; 1Pet 2:4-8
[b]**2:21** 1Kor 3:16-17
[c]**3:1** 2Tim 1:8; Flp 1:1-9
[d]**3:2** Kol 1:25; Rum 1:5; 11:13; 1Kor 4:1; Efe 4:7; Kol 1:25; Mdo 9:15
[e]**3:3** Rum 16:25; 1Kor 2:10
[f]**3:4** 2Kor 11:6; 1Kor 4:1; Efe 6:19
[g]**3:5** Rum 16:26; Mdo 10:28; Rum 16:25; Efe 3:9; 2:20
[h]**3:6** Gal 3:29; Efe 2:15-16
[i]**3:7** 1Kor 3:6; Efe 1:19
[j]**3:8** 1Kor 15:19; 1Tim 1:13, 15; Gal 1:16; 2:8; 1Tim 2:7; 2Tim 1:11; Efe 1:7; Kol 1:27
[k]**3:9** Rum 16:25; Efe 3:3; 1:9; Rum 16:25; 1Kor 2:7; Kol 1:26; Za 33:6
[l]**3:10** 1Kor 2:7; 1Pet 1:12; Efe 6:12
[m]**3:11** Efe 1:9; 1:11
[n]**3:12** Efe 2:18; Kol 3:4
[o]**3:13** Mdo 14:22; Flp 1:14; 1The 3:3; 2Kor 3:4
[p]**3:14** Flp 2:10
[q]**3:15** Efe 1:10; Flp 2:9, 10, 11
[r]**3:16** Kol 1:11; Rum 7:22
[s]**3:17** Yn 14:23; Kol 1:22
[t]**3:19** Kol 2:10; Efe 1:23
[u]**3:20** Rum 16:25; Yud 24; 1Kor 2:9; Kol 1:29; Efe 3:7
[v]**3:21** Rum 11:36; 16:27; Ebr 13:21

Kristo Yesu kwa vizazi vyote, milele na
milele. Amen.

*Umoja Katika Mwili Wa Kristo*

4 [a]Basi, mimi niliye mfungwa wa Bwana,
nawasihi mwenende kama inavyostahili
wito wenu mlioitiwa. 2 [b]Kwa unyenyekevu
wote na upole, mkiwa wavumilivu,
mkichukuliana kwa upendo. 3 [c]Jitahidini
kudumisha umoja wa Roho katika kifungo
cha amani. 4 [d]Kuna mwili mmoja na Roho
mmoja, kama vile mlivyoitwa katika
tumaini moja. 5 [e]Tena kuna Bwana mmoja,
imani moja, ubatizo mmoja, 6 [f]Mungu
mmoja ambaye ni Baba wa wote, aliye juu
ya yote, katika yote na ndani ya yote.
7 [g]Lakini kila mmoja wetu amepewa
neema kwa kadiri ya kipimo cha kipawa
cha Kristo. 8 [h]Kwa hiyo husema:

"Alipopaa juu zaidi, [i]
aliteka mateka,
akawapa wanadamu vipawa."

9 [j](Asemapo "alipaa juu," maana yake nini
isipokuwa ni kusema pia kwamba Kristo
alishuka pande za chini sana za dunia?[k]
10 [l]Yeye aliyeshuka ndiye alipaa juu zaidi
kupita mbingu zote, ili apate kuujaza
ulimwengu wote.) 11 [m]Ndiye aliweka
wengine kuwa mitume, wengine kuwa
manabii, wengine kuwa wainjilisti, wengine
kuwa wachungaji na walimu, 12 [n]kwa
kusudi la kuwakamilisha watakatifu kwa
ajili ya kazi za huduma, ili kwamba mwili
wa Kristo upate kujengwa 13 [o]mpaka sote
tutakapoufikia umoja katika imani na
katika kumjua sana Mwana wa Mungu na
kuwa watu wazima kwa kufikia kimo cha
ukamilifu wa Kristo.
14 [p]Ili tusiwe tena watoto wachanga,
tukitupwatupwa huku na huku na
kuchukuliwa na kila upepo wa mafundisho
kwa hila za watu, kwa ujanja, kwa kufuata
njia zao za udanganyifu. 15 [q]Badala yake,
tukiambiana kweli kwa upendo, katika
mambo yote tukue, hata tumfikie yeye aliye
kichwa, yaani, Kristo. 16 [r]Kutoka kwake,
mwili wote ukiwa umeungamanishwa na
kushikamanishwa pamoja kwa msaada wa
kila kiungo, hukua na kujijenga wenyewe
katika upendo, wakati kila kiungo kinafanya
kazi yake.

*Maisha Ya Zamani Na Maisha Mapya*

17 [s]Hivyo nawaambia hivi, nami nasisitiza
katika Bwana kwamba, msiishi tena kama
watu wa Mataifa waishivyo, katika ubatili
wa mawazo yao. 18 [t]Watu hao akili zao
zimetiwa giza na wametengwa mbali na
uzima wa Mungu kwa sababu ya ujinga
wao kutokana na ugumu wa mioyo yao.
19 [u]Wakiisha kufa ganzi, wamejitia katika
mambo ya ufisadi na kupendelea kila aina
ya uchafu, wakiendelea kutamani zaidi.
20 Lakini ninyi, hivyo sivyo mlivyojifunza
Kristo. 21 [v]Kama hivyo ndivyo ilivyo, ninyi
mmemsikia, tena mmefundishwa naye, vile
kweli ilivyo katika Yesu. 22 [w]Mlifundishwa
kuuvua mwenendo wenu wa zamani, utu
wenu wa kale, ulioharibiwa na tamaa
zake za udanganyifu, 23 [x]ili mfanywe upya

[a]**4:1** Efe 3:1; Kol 1:10; 1The 2:12
[b]**4:2** Kol 3:12, 13; Efe 1:4
[c]**4:3** Kol 3:14; Rum 15:5
[d]**4:4** 1Kor 12:13
[e]**4:5** 1Kor 8:6; 2Kor 11:4; Yud 3; Gal 3:27, 28; Ebr 6:6
[f]**4:6** Rum 11:36; 1Kor 12:6; Mal 2:10; 1Kor 8:6; 12:6; Rum 11:36
[g]**4:7** 1Kor 12:7, 11; Rum 12:3
[h]**4:8** Kol 2:15; Za 68:18
[i]8 Juu zaidi hapa ina maana mbingu za mbingu.
[j]**4:9** Yn 3:13; 6:33, 62
[k]9 Pande za chini sana za dunia hapa maana yake Sheol kwa Kiebrania, yaani Kuzimu.
[l]**4:10** Mdo 1:9, 11; 1Tim 3:16; Ebr 4:14; 7:26; 9:24; Mdo 2:13; Mit 30:1-4; Efe 1:23
[m]**4:11** 2Pet 3:2; Mdo 21:8
[n]**4:12** 1Kor 12:27; 1Pet 2:5; 2Tim 3:17
[o]**4:13** Kol 1:28
[p]**4:14** 1Kor 14:20; Yn 1:6; Efe 6:11
[q]**4:15** Efe 1:22
[r]**4:16** Kol 2:19
[s]**4:17** Rum 1:21
[t]**4:18** Rum 1:21; Efe 2:12; 2Kor 3:14
[u]**4:19** 1Tim 4:2; Rum 1:24; Kol 3:5
[v]**4:21** Efe 1:13
[w]**4:22** 1Pet 2:1; Rum 6:6
[x]**4:23** Kol 3:10

roho na nia zenu, 24 [a]mkajivike utu mpya,
ulioumbwa sawasawa na mfano wa Mungu
katika haki yote na utakatifu.

*Kanuni Za Maisha Mapya*

25 [b]Kwa hiyo kila mmoja wenu avue
uongo na kuambiana kweli mtu na jirani
yake, kwa maana sisi sote tu viungo vya
mwili mmoja. 26 [c]Mkikasirika, msitende
dhambi, wala jua lisichwe mkiwa bado
mmekasirika, 27 [d]wala msimpe ibilisi nafasi.
28 [e]Yeye ambaye amekuwa akiiba, asiibe
tena, lakini lazima ajishughulishe, afanye
kitu kifaacho kwa mikono yake mwenyewe,
ili awe na kitu cha kuwagawia wahitaji.
29 [f]Maneno mabaya yasitoke vinywani
mwenu, bali yale yafaayo kwa ajili ya
kuwajenga wengine kulingana na mahitaji
yao, ili yawafae wale wasikiao. 30 [g]Wala
msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu,
ambaye kwake mlitiwa muhuri kwa ajili
ya siku ya ukombozi. 31 [h]Ondoeni kabisa
uchungu, ghadhabu, hasira, makelele na
masingizio pamoja na kila aina ya uovu.
32 [i]Kuweni wafadhili na wenye kuhurumiana
ninyi kwa ninyi, mkisameheana, kama vile
naye Mungu katika Kristo alivyowasamehe
ninyi.

*Kuenenda Nuruni*

5 [j]Kwa hiyo, mfuateni Mungu kama
watoto wapendwao, 2 [k]mkiishi maisha
ya upendo, kama vile Kristo alivyotupenda
sisi akajitoa kwa ajili yetu kuwa sadaka
yenye harufu nzuri na dhabihu kwa Mungu.
3 [l]Lakini uasherati, usitajwe miongoni
mwenu, wala uchafu wa aina yoyote,
wala tamaa, kwa sababu mambo haya
hayastahili miongoni mwa watakatifu.
4 [m]Wala pasiwepo mazungumzo machafu
ya aibu, au maneno ya upuzi au mzaha,
ambayo hayafai, badala yake mshukuruni
Mungu. 5 [n]Kwa habari ya mambo haya
mjue hakika kwamba: Msherati, wala
mtu mwovu, wala mwenye tamaa mbaya,
mtu kama huyo ni mwabudu sanamu,
kamwe hataurithi Ufalme wa Kristo na wa
Mungu. 6 [o]Mtu yeyote na asiwadanganye
kwa maneno matupu, kwa kuwa hasira
ya Mungu huwaka kwa sababu ya mambo
kama haya juu ya wale wasiomtii. 7 Kwa
hiyo, msishirikiane nao.
8 [p]Kwa maana zamani ninyi mlikuwa giza,
lakini sasa ninyi ni nuru katika Bwana.
Enendeni kama watoto wa nuru 9 [q](kwa
kuwa tunda la nuru hupatikana katika
wema wote, haki na kweli), 10 [r]nanyi tafuteni
yale yanayompendeza Bwana. 11 [s]Msishiriki
matendo ya giza yasiyofaa, bali yafichueni.
12 [t]Kwa maana ni aibu hata kutaja mambo
yale ambayo wasiotii wanayafanya sirini.
13 [u]Lakini kila kitu kilichowekwa nuruni,
huonekana, 14 [v]kwa kuwa nuru ndiyo
hufanya kila kitu kionekane. Hii ndiyo
sababu imesemekana:

"Amka, wewe uliyelala,
ufufuke kutoka kwa wafu,
naye Kristo atakuangazia."

15 Kwa hiyo angalieni sana jinsi
mnavyoenenda, si kama watu wasio
na hekima, bali kama wenye hekima,
16 [w]mkiukomboa wakati, kwa sababu nyakati
hizi ni za uovu. 17 [x]Kwa hiyo msiwe wajinga,

[a]**4:24** Rum 6:4; Efe 2:10
[b]**4:25** Law 19:11; Rum 12:15
[c]**4:26** Za 4:4; Yak 1:19, 20; Mt 5:22
[d]**4:27** Yak 4:7; 1Pet 5:9
[e]**4:28** Mdo 20:35; 1The 4:11; Lk 3:11
[f]**4:29** Kol 3:8; Mt 12:36; Efe 5:4; Kol 3:8; 4:6; 1The 5:11
[g]**4:30** 1The 5:19; Rum 8:23
[h]**4:31** Kol 3:8; Tit 3:2; Yak 4:11; 1Pet 2:1; Tit 3:3
[i]**4:32** Mt 6:14, 15
[j]**5:1** Lk 6:36; Mt 5:45; 8; Lk 6:26; Efe 4:32
[k]**5:2** Gal 1:4; 2Kor 6:15; Ebr 7:27
[l]**5:3** Kol 3:5; 1Kor 6:18; Efe 4:29
[m]**5:4** Mt 12:35; Efe 4:29; Rum 1:28; Kol 3:8
[n]**5:5** Kol 3:5; 1Kor 6:9
[o]**5:6** Rum 1:18; Kol 2:4, 8; Yer 29:8; Mt 24:4; Kol 2:4, 8, 18; 2The 2:3; Rum 1:1
[p]**5:8** Efe 2:2; Yn 8:12
[q]**5:9** Gal 5:22; Mt 7:16-20; Rum 15:14
[r]**5:10** 1Tim 5:4; Rum 12:2; Flp 1:10; 1The 5:21; 1Tim 2:3
[s]**5:11** Rum 13:12; 2Kor 6:14; Yn 16:8
[t]**5:12** Rum 1:24, 26; Efe 5:3
[u]**5:13** Yn 3:20, 21
[v]**5:14** Rum 13:11; Yn 5:25; Isa 60:1
[w]**5:16** Kol 4:5; Efe 6:13
[x]**5:17** Rum 12:2; Kol 1:9

bali mpate kujua nini mapenzi ya Bwana.
18 [a]Pia msilewe kwa mvinyo, ambamo ndani
yake mna upotovu, bali mjazwe Roho.
19 [b]Msemezane ninyi kwa ninyi kwa zaburi,
nyimbo na tenzi za rohoni, mkimwimbia
na kumsifu Bwana mioyoni mwenu, 20 [c]siku
zote mkimshukuru Mungu Baba kwa kila
jambo katika Jina la Bwana wetu Yesu
Kristo.
21 [d]Nyenyekeaneni ninyi kwa ninyi kwa
heshima kwa ajili ya Kristo.

*Mafundisho Kuhusu Wake Na Waume*

22 [e]Ninyi wake, watiini waume zenu kama
kumtii Bwana. 23 [f]Kwa maana mume ni
kichwa cha mkewe kama vile Kristo alivyo
kichwa cha Kanisa, ambalo ni mwili wake,
naye Kristo ni Mwokozi wake. 24 [g]Basi, kama
vile Kanisa linavyomtii Kristo, vivyo hivyo
na wake nao imewapasa kuwatii waume
zao kwa kila jambo.
25 [h]Ninyi waume, wapendeni wake zenu,
kama vile Kristo alivyolipenda Kanisa
akajitoa kwa ajili yake 26 [i]kusudi alifanye
takatifu, akilitakasa kwa kuliosha kwa
maji katika Neno lake, 27 [j]apate kujiletea
Kanisa tukufu lisilo na doa wala kunyanzi
au waa lolote, bali takatifu na lisilo na
hatia. 28 Vivyo hivyo imewapasa waume
kuwapenda wake zao kama miili yao
wenyewe. Ampendaye mkewe hujipenda
mwenyewe. 29 Hakuna mtu anayeuchukia
mwili wake mwenyewe, bali huulisha na
kuutunza vizuri, kama Kristo anavyolitunza
Kanisa lake. 30 [k]Sisi tu viungo vya mwili
wake. 31 [l]"Kwa sababu hii, mwanaume
atamwacha baba yake na mama yake,
naye ataambatana na mkewe, na hao
wawili watakuwa mwili mmoja." 32 Siri
hii ni kubwa, bali mimi nanena kuhusu
Kristo na Kanisa. 33 Hata hivyo, kila mmoja
wenu ampende mkewe kama anavyoipenda
nafsi yake mwenyewe, naye mke lazima
amheshimu mumewe.

*Mafundisho Kuhusu Watoto Na Wazazi*

6 [m]Enyi watoto, watiini wazazi wenu
katika Bwana, kwa kuwa hili ni jema.
2 [n]"Waheshimu baba yako na mama yako,"
hii ndio amri ya kwanza yenye ahadi,
3 [o]"upate baraka na uishi siku nyingi
duniani."
4 [p]Ninyi akina baba, msiwachokoze
watoto wenu, bali waleeni kwa nidhamu
na mafundisho ya Bwana.

*Mafundisho Kuhusu Watumwa Na Mabwana*

5 [q]Ninyi watumwa, watiini hao walio
mabwana zenu hapa duniani kwa heshima
na kwa kutetemeka na kwa moyo mmoja,
kama vile mnavyomtii Kristo. 6 [r]Watiini, si
tu wakati wakiwaona ili mpate upendeleo
wao, bali mtumike kama watumwa wa
Kristo, mkifanya mapenzi ya Mungu kwa
moyo. 7 [s]Tumikeni kwa moyo wote, kama
vile mnamtumikia Bwana na si wanadamu.
8 [t]Mkijua kwamba Bwana atampa kila mtu
thawabu kwa lolote jema alilotenda, kama
yeye ni mtumwa au ni mtu huru.
9 [u]Nanyi mabwana, watendeeni watumwa
wenu kwa jinsi iyo hiyo. Msiwatishe, kwa
kuwa mnajua ya kwamba yeye aliye Bwana
wenu na Bwana wao yuko mbinguni, naye
hana upendeleo.

*Silaha Za Mungu*

10 [v]Hatimaye, mzidi kuwa hodari katika

[a]**5:18** Isa 28:7; Lk 1:15
[b]**5:19** Za 27:6
[c]**5:20** Ay 1:21
[d]**5:21** Gal 5:13; 1Pet 5:5; Flp 2:3
[e]**5:22** Mwa 3:16; Tit 2:5; Efe 6:5
[f]**5:23** 1Kor 11:3; Efe 1:22
[g]**5:24** Kol 3:20; Tit 2:9
[h]**5:25** Kol 3:19
[i]**5:26** Mdo 22:16
[j]**5:27** Efe 1:4; Kol 1:22
[k]**5:30** 1Kor 12:27
[l]**5:31** Mwa 2:24; Mt 19:5
[m]**6:1** Kol 3:20; Mt 6:20
[n]**6:2** Kut 20:12; Kum 5:16; 27:16; Yer 35:18; Eze 22:7; Mal 1:6; Mt 15:4; Mk 7:10
[o]**6:3** Kut 20; 12; Kum 5:16
[p]**6:4** Kol 3:21; Mit 13:24; 22:6
[q]**6:5** Tit 2:9; Kol 3:22; Efe 5:22
[r]**6:6** Rum 6:22; Kol 3:22, 23
[s]**6:7** Kol 3:23
[t]**6:8** Kol 3:24
[u]**6:9** Ay 31:13, 14
[v]**6:10** Hag 2:4; Efe 1:19

Bwana na katika uweza wa nguvu zake.
11 [a]Vaeni silaha zote za Mungu ili kwamba
mweze kuzipinga hila za ibilisi. 12 [b]Kwa
maana kushindana kwetu si juu ya nyama
na damu, bali dhidi ya falme, mamlaka,
dhidi ya wakuu wa giza na majeshi ya
pepo wabaya katika ulimwengu wa roho.
13 [c]Kwa hiyo vaeni silaha zote za Mungu
ili mweze kushindana siku ya uovu
itakapokuja nanyi mkiisha kufanya yote,
simameni imara. 14 [d]Kwa hiyo simameni
imara mkiwa mmejifunga kweli kiunoni na
kuvaa dirii ya haki kifuani, 15 [e]nayo miguu
yenu ifungiwe utayari tuupatao kwa Injili
ya amani. 16 [f]Zaidi ya haya yote, twaeni
ngao ya imani, ambayo kwa hiyo mtaweza
kuizima mishale yote yenye moto ya yule
mwovu. 17 [g]Vaeni chapeo ya wokovu na
mchukue upanga wa Roho, ambao ni Neno
la Mungu. 18 [h]Mkiomba kwa Roho siku zote
katika sala zote na maombi, mkikesha kila
wakati mkiwaombea watakatifu wote.

19 [i]Niombeeni na mimi pia, ili kila
nifunguapo kinywa changu, nipewe maneno
ya kusema, niweze kutangaza siri ya Injili
kwa ujasiri, 20 [j]ambayo mimi ni balozi wake
katika vifungo. Ombeni ili nipate kuhubiri
kwa ujasiri kama inipasavyo.

### *Salamu Za Mwisho*

21 [k]Tikiko, aliye ndugu mpendwa na
mtumishi mwaminifu katika Bwana,
atawaambia kila kitu, ili pia mpate kujua
hali yangu na kile ninachofanya sasa.
22 [l]Ninamtuma kwenu kwa ajili ya kusudi
hili hasa, ili mpate kujua hali yetu, na
awatie moyo.

23 [m]Amani iwe kwa ndugu, na pendo
pamoja na imani kutoka kwa Mungu Baba
na Bwana Yesu Kristo. 24 [n]Neema iwe na
wote wampendao Bwana wetu Yesu Kristo
kwa upendo wa dhati. Amen.

---

[a]**6:11** Rum 13:12
[b]**6:12** Efe 1:21; Rum 8:38; Efe 1:3
[c]**6:13** Efe 6:11; 2Kor 6:7; 10:4, 11; Efe 5:16
[d]**6:14** Isa 1:5; Za 132:9
[e]**6:15** Isa 52:7; Rum 10:15
[f]**6:16** 1Yn 5:4; Mt 5:37
[g]**6:17** Isa 59:17; Ebr 4:12
[h]**6:18** Lk 18:1; Mt 26:41; Flp 4:6
[i]**6:19** 1The 5:25; Mdo 4:29; 2Kor 3:12
[j]**6:20** 2Kor 5:20; Mdo 21:23
[k]**6:21** Mdo 20:4
[l]**6:22** Kol 4:7-9
[m]**6:23** Gal 6:16; 1Pet 5:14
[n]**6:24** Tit 2:7; 1Pet 1:8

# WAFILIPI

*Salamu*

1 [a]Waraka wa Paulo na Timotheo,
watumishi wa Kristo Yesu:
Kwa watakatifu wote katika Kristo Yesu
walioko Filipi, pamoja na waangalizi na
mashemasi:
2 [b]Neema na amani itokayo kwa Mungu
Baba yetu na kwa Bwana wetu Yesu Kristo
iwe nanyi.

*Shukrani Na Maombi*

3 [c]Ninamshukuru Mungu wangu kila
niwakumbukapo ninyi. 4 [d]Katika maombi
yangu yote daima nimekuwa nikiwaombea
ninyi nyote kwa furaha, 5 [e]kwa sababu ya
kushiriki kwenu katika kueneza Injili,
tangu siku ya kwanza hadi leo. 6 [f]Nina
hakika kwamba yeye aliyeianza kazi
njema mioyoni mwenu, ataiendeleza na
kuikamilisha hata siku ya Kristo Yesu.
7 [g]Ni haki na ni wajibu wangu kufikiri
hivi juu yenu nyote, kwa sababu ninyi
mko moyoni mwangu. Ikiwa nimefungwa
au nikiwa ninaitetea na kuithibitisha Injili,
ninyi nyote mnashiriki neema ya Mungu
pamoja nami. 8 [h]Mungu ni shahidi wangu
jinsi ninavyowaonea shauku ninyi nyote
kwa huruma ya Kristo Yesu.
9 [i]Haya ndiyo maombi yangu: kwamba
upendo wenu uongezeke zaidi na zaidi
katika maarifa na ufahamu wote, 10 [j]ili
mpate kutambua yale yaliyo mema, mkawe
safi, wasio na hatia hadi siku ya Kristo,
11 [k]mkiwa mmejawa na matunda ya haki
yapatikanayo kwa njia ya Yesu Kristo, kwa
utukufu na sifa za Mungu.

*Kufungwa Kwa Paulo Kwaieneza Injili*

12 [l]Basi, ndugu zangu, nataka mjue
kwamba mambo yale yaliyonipata kwa
kweli yamesaidia sana kueneza Injili.
13 [m]Matokeo yake ni kwamba imejulikana
wazi kwa walinzi wote wa jumba la kifalme
na kwa wengine wote kuwa nimefungwa
kwa ajili ya Kristo. 14 [n]Kwa sababu ya
vifungo vyangu, ndugu wengi katika Bwana
wametiwa moyo kuhubiri neno la Mungu
kwa ujasiri zaidi na bila woga.
15 [o]Ni kweli kwamba wengine
wanamhubiri Kristo kutokana na wivu na
kwa kutaka kushindana, lakini wengine
wanamhubiri Kristo kwa nia njema. 16 [p]Hawa
wa mwisho wanamhubiri Kristo kwa moyo
wa upendo, wakifahamu kwamba nimo
humu gerezani kwa ajili ya kuitetea Injili.
17 [q]Hao wa kwanza wanamtangaza Kristo
kutokana na tamaa zao wenyewe wala
si kwa moyo mweupe, bali wanakusudia
kuongeza mateso yangu katika huku
kufungwa kwangu. 18 [r]Lakini inadhuru nini?
Jambo la muhimu ni kwamba kwa kila njia,
ikiwa ni kwa nia mbaya au njema, Kristo
anahubiriwa. Nami kwa ajili ya jambo hilo
ninafurahi.
Naam, nami nitaendelea kufurahi,
19 [s]kwa maana ninajua kwamba kwa
maombi yenu na kwa msaada unaotolewa
na Roho wa Yesu Kristo, yale yaliyonipata
mimi yatageuka kuwa wokovu wangu.

---

[a]**1:1** Mdo 16:1; 2Kor 1:1; Mdo 9:13; 16:12; 1Tim 3:1; 3:8
[b]**1:2** Rum 1:7; 1Kor 1:2; 1Pet 1:2
[c]**1:3** Rum 1:8; 1Kor 1:6, 8; Efe 1:15, 16; 1Kor 1:4; Kol 1:3; 1The 1:2
[d]**1:4** Rum 1:10
[e]**1:5** Mdo 2:42; Flp 4:15; Mdo 16:12-40
[f]**1:6** Flp 2:13; 1Kor 16:8; Za 138:8
[g]**1:7** 2Pet 1:13; 2Kor 7:3; Flp 1:13, 14, 17; Mdo 21:33
[h]**1:8** Rum 1:9; 2Kor 1:23; 1The 2:5
[i]**1:9** 1The 3:12
[j]**1:10** 1Kor 1:8; Rum 2:18; Efe 5:10; Mdo 24:16; 1The 3:13; 5:23
[k]**1:11** Yak 3:18; Yn 15:4; Efe 2:10; Kol 1:16; Yn 15:8; Efe 1:12, 14
[l]**1:12** 2Tim 2:9
[m]**1:13** Mdo 21:33
[n]**1:14** Mdo 21:33
[o]**1:15** Flp 2:3
[p]**1:16** Flp 1:7, 12
[q]**1:17** Flp 2:3; Mdo 21:33
[r]**1:18** Flp 2:17, 18
[s]**1:19** 2Kor 1:11; Mdo 16:7; 16:23

20 [a]Ninatarajia kwa shauku kubwa na
kutumaini kwamba sitaaibika kwa njia
yoyote, bali nitakuwa na ujasiri wa kutosha
ili sasa kama wakati mwingine wowote,
Kristo atukuzwe katika mwili wangu, ikiwa
ni kwa kuishi au kwa kufa. 21 [b]Kwa maana
kwangu mimi, kuishi ni Kristo, na kufa ni
faida. 22 [c]Kama nitaendelea kuishi katika
mwili, kwangu hili ni kwa ajili ya matunda
ya kazi. Lakini sijui nichague lipi? Mimi
sijui! 23 [d]Ninavutwa kati ya mambo mawili:
Ninatamani kuondoka nikakae pamoja na
Kristo, jambo hilo ni bora zaidi. 24 Lakini
kwa sababu yenu ni muhimu zaidi mimi
nikiendelea kuishi katika mwili. 25 [e]Kwa
kuwa nina matumaini haya, ninajua
kwamba nitaendelea kuwepo na kuwa
pamoja nanyi nyote, ili mpate kukua na
kuwa na furaha katika imani. 26 [f]Ili kwamba
furaha yenu iwe nyingi katika Kristo Yesu
kwa ajili yangu kwa kule kuja kwangu
kwenu tena.

*Kuenenda Ipasavyo Injili*

27 [g]Lakini lolote litakalotukia, mwenende
kama ipasavyo Injili ya Kristo, ili kwamba
nikija na kuwaona au ikiwa sipo, nipate
kusikia haya juu yenu: Kuwa mnasimama
imara katika roho moja, mkiishindania
imani ya Injili kwa umoja, 28 [h]wala
msitishwe na wale wanaowapinga. Hii ni
ishara kwao kuwa wataangamia, lakini
ninyi mtaokolewa, na hii ni kazi ya Mungu.
29 [i]Kwa maana mmepewa kwa ajili ya
Kristo, si kumwamini tu, bali pia kuteswa
kwa ajili yake, 30 [j]kwa kuwa mnashiriki
mashindano yale yale mliyoyaona nikiwa
nayo na ambayo hata sasa mnasikia kuwa
bado ninayo.

*Kuiga Unyenyekevu Wa Kristo*

2 [k]Kama kukiwa na jambo lolote la kutia
moyo katika kuunganishwa na Kristo,
kukiwa faraja yoyote katika upendo wake,
kukiwa na ushirika wowote na Roho,
kukiwa na wema wowote na huruma, 2 [l]basi
ikamilisheni furaha yangu kwa kuwa na
nia moja, mkiwa na upendo huo moja,
mkiwa wa roho na kusudi moja. 3 [m]Msitende
jambo lolote kwa nia ya kujitukuza wala
kujivuna, bali kwa unyenyekevu kila mtu
amhesabu mwingine bora kuliko nafsi yake.
4 [n]Kila mmoja wenu asiangalie faida yake
mwenyewe tu, bali pia ajishughulishe kwa
faida ya wengine.

5 [o]Kuweni na nia ile ile aliyokuwa nayo
Kristo Yesu:

6 [p]Yeye, ingawa alikuwa na asili ya
Mungu hasa,
hakuona kule kuwa sawa na
Mungu
kuwa kitu cha kushikilia,
7 [q]bali alijifanya si kitu,
akachukua hali hasa na mtumwa,
naye akazaliwa katika umbo la
mwanadamu.
8 [r]Naye akiwa na umbo la
mwanadamu,
alijinyenyekeza, akatii hata mauti:
naam, mauti ya msalaba!
9 [s]Kwa hiyo, Mungu alimtukuza juu
sana,
na kumpa Jina lililo kuu kuliko
kila jina,
10 [t]ili kwa Jina la Yesu, kila goti
lipigwe,
la vitu vya mbinguni, na vya
duniani,
na vya chini ya nchi,

---

[a]**1:20** Rum 8:19; 1Kor 6:20; Rum 14:8
[b]**1:21** Gal 2:20
[c]**1:22** Rum 1:13
[d]**1:23** 2Tim 4:6; Yn 12:26; 2Kor 5:8
[e]**1:25** Flp 2:24
[f]**1:26** 2Kor 1:14; 5:12
[g]**1:27** Efe 4:1; 1Kor 16:13; Yud 3
[h]**1:28** 2The 1:5; Rum 8:17; 2Tim 2:11
[i]**1:29** Mt 5:11, 12; Mdo 5:41; 14:22
[j]**1:30** Kol 2:1; Ebr 10:32; Mdo 16:19-40
[k]**2:1** 2Kor 13:14; Kol 3:12
[l]**2:2** Yn 3:29; Flp 4:2; Rum 12:16; 15:15
[m]**2:3** Gal 5:26; Rum 12:10; 1Pet 5:5
[n]**2:4** 1Kor 10:24, 33; 13:5
[o]**2:5** Mt 11:29; Yn 13:15; 1Pet 2:21; 1Yn 2:6
[p]**2:6** Yn 1:1; 5:18
[q]**2:7** Mt 20:28; Rum 8:3; Ebr 5:8
[r]**2:8** Rum 5:19; Ebr 5:8
[s]**2:9** Dan 7:14; Mdo 2:33; Efe 1:20
[t]**2:10** Rum 14:11; Efe 1:10

11 [a]na kila ulimi ukiri ya kwamba
Yesu Kristo ni Bwana,
kwa utukufu wa Mungu Baba.

*Ng'aeni Kama Mianga Katika Ulimwengu*

12 [b]Kwa hiyo, wapenzi wangu, kama vile
ambavyo mmekuwa mkitii siku zote, si
tu wakati nikiwa pamoja nanyi, bali sasa
zaidi sana nisipokuwepo, utimizeni wokovu
wenu kwa kuogopa na kutetemeka, 13 [c]kwa
maana Mungu ndiye atendaye kazi ndani
yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu kwa
kulitimiza kusudi lake jema.
14 [d]Fanyeni mambo yote bila kunung'unika
wala kushindana, 15 [e]ili msiwe na lawama
wala hatia, bali mwe wana wa Mungu wasio
na kasoro katika kizazi chenye ukaidi na
kilichopotoka, ambacho ndani yake ninyi
mnang'aa kama mianga ulimwenguni.
16 [f]Mkilishika neno la uzima, ili nipate kuona
fahari siku ya Kristo kwamba sikupiga mbio
wala kujitaabisha bure. 17 [g]Lakini hata kama
nikimiminwa kama sadaka ya kinywaji
kwenye dhabihu na huduma itokayo katika
imani yenu, mimi ninafurahi na kushangilia
pamoja nanyi nyote. 18 [h]Vivyo hivyo, ninyi
nanyi imewapasa kufurahi na kushangilia
pamoja nami.

*Paulo Amsifu Timotheo*

19 [i]Natumaini katika Bwana Yesu kumtuma
Timotheo hivi karibuni aje kwenu, ili nipate
kufarijika moyo nitakapopata habari zenu.
20 [j]Sina mtu mwingine kama yeye, ambaye
ataangalia hali yenu kwa halisi. 21 [k]Kwa
maana kila mmoja anajishughulisha zaidi
na mambo yake mwenyewe wala si yale
ya Yesu Kristo. 22 [l]Lakini ninyi wenyewe
mnajua jinsi Timotheo alivyojithibitisha
mwenyewe, kwa maana ametumika pamoja
nami kwa kazi ya Injili, kama vile mwana
kwa baba yake. 23 [m]Kwa hiyo, ninatumaini
kumtuma kwenu upesi mara nitakapojua
mambo yangu yatakavyokuwa. 24 [n]Nami
mwenyewe ninatumaini katika Bwana
kwamba nitakuja kwenu hivi karibuni.

*Paulo Amsifu Epafrodito*

25 [o]Lakini nadhani ni muhimu kumtuma
tena kwenu Epafrodito, ndugu yangu na
mtendakazi pamoja nami, aliye askari
mwenzangu, ambaye pia ni mjumbe wenu
mliyemtuma ili ashughulike na mahitaji
yangu. 26 [p]Kwa maana amekuwa akiwaonea
sana shauku ninyi nyote, akiwa na wasiwasi
kwa kuwa mlisikia kwamba alikuwa
mgonjwa. 27 Kweli alikuwa mgonjwa,
tena karibu ya kufa. Lakini Mungu
alimhurumia, wala si yeye tu, bali hata na
mimi alinihurumia, nisipatwe na huzuni
juu ya huzuni. 28 [q]Kwa hiyo mimi ninafanya
bidii kumtuma kwenu ili mtakapomwona
kwa mara nyingine, mpate kufurahi, nami
wasiwasi wangu upungue. 29 [r]Kwa hiyo
mpokeeni katika Bwana kwa furaha kubwa,
nanyi wapeni heshima watu kama hawa,
30 [s]kwa sababu alikaribia kufa kwa ajili ya
kazi ya Kristo, akihatarisha maisha yake ili
aweze kunihudumia vile ninyi hamkuweza.

*Hakuna Tumaini Katika Mwili*

3 [t]Hatimaye, ndugu zangu, furahini katika
Bwana! Mimi kuwaandikia mambo yale
yale hakuniudhi, kwa maana ni kinga kwa
ajili yenu.
2 [u]Jihadharini na mbwa, wale watenda
maovu, jihadharini na wale wajikatao
miili yao, wasemao ili kuokoka ni lazima

[a]**2:11** Yn 13:13; Mdo 2:36; Rum 14:9; 1Kor 8:6; 12:3
[b]**2:12** 2Kor 7:15; 1Pet 1:17; Za 2:11
[c]**2:13** Ezr 1:5; Yn 15:5; 2Kor 3:5; 1The 2:11
[d]**2:14** 1Kor 10:10; 1Pet 4:9
[e]**2:15** Mt 5:45, 48; Efe 5:1; Mdo 2:40
[f]**2:16** 1The 2:19
[g]**2:17** 2Tim 4:6; Rum 15:16
[h]**2:18** Flp 3:1; 4:4
[i]**2:19** Mdo 16:1; Flp 2:23
[j]**2:20** 1Kor 16:10
[k]**2:21** 1Kor 10:24; 13:5
[l]**2:22** 1Kor 4:17; 1Tim 1:2
[m]**2:23** Flp 2:19
[n]**2:24** Flp 1:25
[o]**2:25** Flp 1:1
[p]**2:26** Flp 1:8
[q]**2:28** Flp 2:25
[r]**2:29** 1Kor 16:18; 1Tim 5:17
[s]**2:30** 1Kor 16:17
[t]**3:1** Flp 2:18; 4:4
[u]**3:2** Za 22:16, 20

kutahiriwa. 3 [a]Kwa maana sisi ndio tulio
tohara, sisi tumwabuduo Mungu katika
Roho, tunaona fahari katika Kristo Yesu,
ambao hatuweki tumaini letu katika mwili,
4 [b]ingawa mimi mwenyewe ninazo sababu
za kuutumainia mwili.

Kama mtu yeyote akidhani anazo
sababu za kuutumainia mwili, mimi
zaidi. 5 [c]Nilitahiriwa siku ya nane, mimi
ni Mwisraeli wa kabila la Benyamini,
Mwebrania wa Waebrania. Kwa habari
ya sheria, ni Farisayo, 6 [d]kwa habari ya
juhudi, nilikuwa nalitesa kanisa, kuhusu
haki ipatikanayo kwa sheria, mimi nilikuwa
sina hatia.

7 [e]Lakini mambo yale yaliyokuwa faida
kwangu, sasa nayahesabu kuwa hasara
kwa ajili ya Kristo. 8 [f]Zaidi ya hayo,
nayahesabu mambo yote kuwa hasara tupu
nikiyalinganisha na faida kubwa ipitayo
kiasi cha kumjua Kristo Yesu Bwana wangu,
ambaye kwa ajili yake nimepata hasara ya
mambo yote, nikiyahesabu kuwa kama mavi
ili nimpate Kristo. 9 [g]Nami nionekane mbele
zake bila kuwa na haki yangu mwenyewe
ipatikanayo kwa sheria, bali ile ipatikanayo
kwa imani katika Kristo, haki ile itokayo
kwa Mungu kwa njia ya imani. 10 [h]Nataka
nimjue Kristo na uweza wa kufufuka kwake
na ushirika wa mateso yake, ili nifanane
naye katika mauti yake, 11 [i]ili kwa njia
yoyote niweze kufikia ufufuo wa wafu.

*Kukaza Mwendo Ili Kufikia Lengo*

12 Si kwamba nimekwisha kufikia, au
kwamba nimekwisha kuwa mkamilifu, la
hasha! Bali nakaza mwendo ili nipate kile
ambacho kwa ajili yake, nimeshikwa na
Kristo Yesu. 13 [j]Ndugu zangu, sijihesabu
kuwa nimekwisha kushika. Lakini ninafanya
jambo moja: Ninasahau mambo yale
yaliyopita, nakaza mwendo kufikia yale
yaliyo mbele. 14 [k]Nakaza mwendo nifikie
ile alama ya ushindi iliyowekwa ili nipate
tuzo ya mwito mkuu wa Mungu ambao
nimeitiwa huko juu mbinguni katika Kristo
Yesu.

15 [l]Hivyo sisi sote tuliokuwa kiroho
tuwaze jambo hili, hata mkiwaza mengine
katika jambo lolote, Mungu ataliweka wazi
hilo nalo. 16 [m]Lakini na tushike sana lile
ambalo tumekwisha kulifikia.

17 [n]Ndugu zangu, kwa pamoja fuateni
mfano wangu na kuwatazama wale
wanaofuata kielelezo tulichowawekea.
18 [o]Kwa maana, kama nilivyokwisha
kuwaambia mara nyingi kabla, nami sasa
nasema tena hata kwa machozi, watu wengi
wanaishi kama adui wa msalaba wa Kristo.
19 [p]Mwisho wa watu hao ni maangamizi,
Mungu wao ni tumbo, na utukufu wao ni
aibu, na mawazo yao yamo katika mambo
ya dunia. 20 [q]Lakini uenyeji wetu uko
mbinguni. Nasi tunamngoja kwa shauku
Mwokozi kutoka huko, yaani, Bwana Yesu
Kristo, 21 [r]atakayeubadili mwili wetu wa
unyonge, ili upate kufanana na mwili wake
wa utukufu, kwa uweza ule ambao kwa huo
aweza hata kuvitiisha vitu vyote chini yake.

4 [s]Kwa hiyo, ndugu zangu, ninaowapenda
na ambao ninawaonea shauku, ninyi
mlio furaha yangu na taji yangu, hivi
ndivyo iwapasavyo kusimama imara katika
Bwana, ninyi wapenzi wangu.

*Mausia*

2 [t]Nawasihi Euodia na Sintike wawe na
nia moja katika Bwana. 3 [u]Naam, nakusihi

[a]**3:3** Gal 3:15; Kol 2:11
[b]**3:4** 2Kor 11:21; 11:8, 22
[c]**3:5** Lk 1:59; 2Kor 11:22; Rum 11:1; Mdo 23:6
[d]**3:6** Mdo 8:3; Rum 10:5
[e]**3:7** Mt 13:44; Lk 14:33
[f]**3:8** Yer 9:23, 24; Yn 17:3
[g]**3:9** Rum 10:5; 9:30
[h]**3:10** Rum 8:17; 6:3-5
[i]**3:11** Yn 11:24; Rum 6:5; Ufu 20:5, 6
[j]**3:13** Lk 9:22
[k]**3:14** Ebr 6:1; 1Kor 9:24; Rum 8:28
[l]**3:15** 1Kor 2:6; Gal 5:10; Efe 1:17; 1The 4:9
[m]**3:16** Gal 6:16; Rum 12:16; 15:15; Flp 2:2
[n]**3:17** 1Kor 4:16; Tit 3:12
[o]**3:18** Mdo 20:31; Gal 6:12
[p]**3:19** Za 73:17; Rum 16:18; 5:21; Yud 13; Rum 8:5, 6; Kol 3:2
[q]**3:20** Efe 2:19; Kol 3:1; Ebr 12:22; 1Kor 1:7
[r]**3:21** Efe 1:19; 1Kor 15:43-53; Rum 8:29; Kol 3:4
[s]**4:1** Flp 1:8; 1Kor 16:13
[t]**4:2** Flp 2:2; 3:16
[u]**4:3** Flp 2:25; Ufu 20:12

wewe pia, mwenzangu mwaminifu,
uwasaidie hawa wanawake, kwa sababu
walijitaabisha katika kazi ya Injili pamoja
nami bega kwa bega, wakiwa pamoja na
Klementi na watendakazi wenzangu ambao
majina yao yameandikwa katika kitabu cha
uzima.
4 [a]Furahini katika Bwana siku zote,
tena nasema furahini! 5 [b]Upole wenu na
ujulikane na watu wote. Bwana yu karibu.
6 [c]Msijisumbue kwa jambo lolote, bali katika
kila jambo kwa kuomba na kusihi pamoja
na kushukuru, haja zenu na zijulikane na
Mungu. 7 [d]Nayo amani ya Mungu, inayopita
fahamu zote, itailinda mioyo yenu na nia
zenu katika Kristo Yesu.
8 [e]Hatimaye, ndugu zangu, mambo yote
yaliyo ya kweli, yoyote yaliyo na sifa
njema, yoyote yaliyo ya haki, yoyote yaliyo
safi, yoyote ya kupendeza, yoyote yenye
staha, ukiwepo uzuri wowote, pakiwepo
chochote kinachostahili kusifiwa, tafakarini
mambo hayo. 9 [f]Mambo yote mliyojifunza
au kuyapokea au kuyasikia kutoka kwangu,
au kuyaona kwangu, yatendeni hayo. Naye
Mungu wa amani atakuwa pamoja nanyi.

*Shukrani Kwa Matoleo Yenu*

10 [g]Nina furaha kubwa katika Bwana
kwamba hatimaye mmeanza upya
kushughulika tena na maisha yangu. Kweli
mmekuwa mkinifikiria lakini mlikuwa
hamjapata nafasi ya kufanya hivyo.
11 [h]Sisemi hivyo kwa vile nina mahitaji, la!
Kwa maana nimejifunza kuridhika katika
hali yoyote. 12 [i]Ninajua kupungukiwa, pia
ninajua kuwa na vingi. Nimejifunza siri
ya kuridhika katika kila hali, wakati wa
kushiba na wakati wa kuona njaa, wakati wa
kuwa na vingi na wakati wa kupungukiwa.
13 [j]Naweza kuyafanya mambo yote katika
yeye anitiaye nguvu.
14 [k]Lakini, mlifanya vyema kushiriki
nami katika taabu zangu. 15 [l]Zaidi ya
hayo, ninyi Wafilipi mnajua kwamba
siku za kwanza nilipoanza kuhubiri Injili,
nilipoondoka Makedonia, hakuna kanisa
jingine lililoshiriki nami katika masuala ya
kutoa na kupokea isipokuwa ninyi. 16 [m]Kwa
maana hata nilipokuwa huko Thesalonike,
mliniletea msaada kwa ajili ya mahitaji
yangu zaidi ya mara moja. 17 [n]Si kwamba
natafuta sana yale matoleo, bali natafuta
sana ile faida itakayozidi sana kwa upande
wenu. 18 [o]Nimelipwa kikamilifu hata na
zaidi; nimetoshelezwa kabisa sasa, kwa
kuwa nimepokea kutoka kwa Epafrodito
vile vitu mlivyonitumia, sadaka yenye
harufu nzuri, dhabihu inayokubalika na ya
kumpendeza Mungu. 19 [p]Naye Mungu wangu
atawajaza ninyi na kila mnachohitaji kwa
kadiri ya utajiri wake katika utukufu ndani
ya Kristo Yesu.
20 [q]Mungu wetu aliye Baba yetu apewe
utukufu milele na milele. Amen.

*Salamu Za Mwisho*

21 [r]Msalimuni kila mtakatifu katika
Kristo Yesu. Ndugu walioko pamoja
nami wanawasalimu. 22 [s]Watakatifu
wote wanawasalimu, hasa wale watu wa
nyumbani mwa Kaisari.
23 [t]Neema ya Bwana Yesu Kristo iwe
pamoja na roho zenu. Amen.

---

[a]**4:4** Za 85:6; 97:12; Hab 3:18; Mt 5:12; Rum 12:12; Flp 3:1
[b]**4:5** Za 119:151; 145:18; Ebr 10:37; Yak 5:8, 9
[c]**4:6** Mt 6:25-34; Kol 4:2; 1Pet 5:7; Za 145:18; Efe 6:18; 1Tim 2:1
[d]**4:7** Isa 26:3; Yn 14:27; Efe 3:19
[e]**4:8** 1The 5:22; Rum 12:17
[f]**4:9** 1Kor 4:16; Rum 12:17
[g]**4:10** 2Kor 11:9
[h]**4:11** 1Tim 6:6, 8; Ebr 13:5
[i]**4:12** 1Kor 4:11; 2Kor 11:9
[j]**4:13** 2Kor 12:9; Efe 3:16; Kol 1:11; 1Tim 1:12; 2Tim 4:17
[k]**4:14** Flp 1:7
[l]**4:15** Flp 1:5; Mdo 16:9; 2Kor 11:8, 9
[m]**4:16** Mdo 17:1; 1The 2:9
[n]**4:17** 1Kor 9:11, 12
[o]**4:18** Flp 2:25; 2Kor 2:14
[p]**4:19** Za 23:1; 2Kor 9:8; Rum 2:4
[q]**4:20** Gal 1:4; 1The 1:3; 3:11, 13; Rum 11:36
[r]**4:21** Gal 1:2
[s]**4:22** Mdo 9:13
[t]**4:23** Rum 16:20; Gal 6:18

# WAKOLOSAI

*Salamu*

1 [a]Paulo, mtume wa Kristo Yesu, kwa
mapenzi ya Mungu, na Timotheo ndugu
yetu:
2 [b]Kwa ndugu watakatifu na waaminifu
katika Kristo, waishio Kolosai:
Neema na amani zitokazo kwa Mungu
Baba yetu ziwe nanyi.

*Shukrani Na Maombi*

3 [c]Siku zote tunamshukuru Mungu,
Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo,
tunapowaombea ninyi, 4 [d]kwa sababu
tumesikia kuhusu imani yenu katika
Kristo Yesu, na upendo wenu mlio nao
kwa watakatifu wote: 5 [e]imani na upendo
ule utokao katika tumaini mlilowekewa
akiba mbinguni, na ambalo mmesikia
habari zake katika neno la kweli, yaani,
ile Injili 6 [f]iliyowafikia ninyi. Duniani kote
Injili hii inazaa matunda na kuenea kama
ilivyokuwa kwenu tangu siku ile mlipoisikia
na kuielewa neema ya Mungu katika kweli
yote. 7 [g]Mlijifunza habari zake kutoka kwa
Epafra, mtumishi mwenzetu mpendwa,
yeye aliye mhudumu mwaminifu wa Kristo
kwa ajili yenu, 8 [h]ambaye pia ametuambia
kuhusu upendo wenu katika Roho.
9 [i]Kwa sababu hii, tangu siku ile
tuliposikia habari zenu, hatujakoma
kuomba kwa ajili yenu na kumsihi Mungu
awajaze ninyi maarifa ya mapenzi yake
katika hekima yote ya kiroho na ufahamu.
10 [j]Nasi tunaomba haya ili mpate kuishi
maisha yanayostahili mbele za Bwana,
na mpate kumpendeza kwa kila namna:
mkizaa matunda kwa kila kazi njema,
mkikua katika kumjua Mungu, 11 [k]mkiwa
mmetiwa nguvu kwa uwezo wote kwa kadiri
ya nguvu yake yenye utukufu, ili mpate
kuwa na wingi wa saburi na uvumilivu.
Nanyi kwa furaha 12 [l]mkimshukuru Baba,
ambaye amewastahilisha kushiriki katika
urithi wa watakatifu katika ufalme wa nuru.
13 [m]Kwa maana ametuokoa kutoka ufalme
wa giza na kutuingiza katika ufalme wa
Mwana wake mpendwa, 14 [n]ambaye katika
yeye tunao ukombozi, yaani msamaha wa
dhambi.

*Ukuu Wa Kristo*

15 [o]Yeye ni mfano wa Mungu asiyeonekana,
mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote.
16 [p]Kwake yeye vitu vyote vilivyoko
mbinguni na juu ya nchi viliumbwa: vitu
vinavyoonekana na visivyoonekana, viwe ni
viti vya enzi au falme, au wenye mamlaka
au watawala; vitu vyote viliumbwa na
yeye na kwa ajili yake. 17 [q]Yeye alikuwepo
kabla ya vitu vyote, na katika yeye vitu
vyote vinashikamana pamoja. 18 [r]Yeye ndiye
kichwa cha mwili, yaani kanisa, naye ndiye
mwanzo na mzaliwa wa kwanza kutoka kwa
wafu, ili yeye awe mkuu katika vitu vyote.
19 [s]Kwa kuwa ilimpendeza Mungu kwamba
utimilifu wake wote ukae ndani yake,
20 [t]na kwa njia yake aweze kuvipatanisha
vitu vyote na yeye mwenyewe, viwe ni
vitu vilivyo duniani au vilivyo mbinguni,

---

[a]**1:1** 1Kor 1:1; 2Kor 1:1; Mdo 16:1
[b]**1:2** Kol 4:18; Rum 1:7
[c]**1:3** Rum 1:8
[d]**1:4** Gal 5:6; Mdo 9:13; Efe 1:15; Flm 5
[e]**1:5** Kol 1:23; 1The 5:8; Tit 1:2; 1Pet 1:4; 2Tim 2:15
[f]**1:6** Kol 1:23; Rum 10:18; Yn 15:16
[g]**1:7** Kol 4:12; Flm 23; Kol 4:7
[h]**1:8** Rum 15:30
[i]**1:9** Kol 1:4; Efe 1:15; Rum 1:10; Efe 5:17
[j]**1:10** Efe 4:1; 2Kor 5:9; Kol 1:6
[k]**1:11** Flp 4:13; Efe 4:2
[l]**1:12** Efe 5:20; Mdo 20:32; 26:18
[m]**1:13** Mdo 26:13; 2Pet 1:11; Mt 3:17
[n]**1:14** Rum 3:24; Efe 1:7
[o]**1:15** Yn 14:9; 1:18; 1Tim 1:17; Ebr 11:27; Kol 1:18
[p]**1:16** Yn 1:3; Efe 1:20, 21; Rum 11:36
[q]**1:17** Yn 1:2
[r]**1:18** Efe 1:22; Kol 1:24; 1Kor 12:27; Za 89:27; Rum 8:29
[s]**1:19** Efe 1:15; Yn 1:16
[t]**1:20** Rum 5:10; Efe 1:10; Lk 2:14; Efe 2:13

kwa kufanya amani kwa damu yake,
iliyomwagika msalabani.
21 [a]Hapo kwanza mlikuwa mmetengana
na Mungu, na mlikuwa adui zake katika nia
zenu kwa sababu ya mienendo yenu mibaya.
22 [b]Lakini sasa Mungu amewapatanisha
ninyi kwa njia ya mwili wa Kristo kupitia
mauti, ili awalete mbele zake mkiwa
watakatifu, bila dosari wala lawama,
23 ikiwa mnaendelea katika imani yenu
mkiwa imara na thabiti, pasipo kuliacha
tumaini lililoahidiwa katika Injili. Hii ndiyo
ile Injili mliyoisikia, ambayo imehubiriwa
kwa kila kiumbe chini ya mbingu, na
ambayo mimi Paulo nimekuwa mtumwa
wake.

*Taabu Ya Paulo Kwa Ajili Ya Kanisa*

24 [c]Sasa nafurahia kule kuteseka kwangu
kwa ajili yenu, na katika mwili wangu
ninatimiliza yale yaliyopungua katika
mateso ya Kristo kwa ajili ya mwili wake,
ambao ni kanisa. 25 [d]Mimi nimekuwa
mtumishi wa kanisa kwa wajibu alionipa
Mungu ili kuwaletea ninyi Neno la Mungu
kwa ukamilifu: 26 [e]Hii ni siri iliyokuwa
imefichika tangu zamani na kwa vizazi
vingi, lakini sasa imefunuliwa kwa
watakatifu. 27 [f]Kwao, Mungu amechagua
kujulisha miongoni mwa watu wa Mataifa
utukufu wa utajiri wa siri hii, ambayo ni
Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu.
28 [g]Yeye ndiye tunayemtangaza,
tukimwonya kila mtu na kumfundisha
kila mtu kwa hekima yote ili tuweze
kumleta kila mmoja akiwa amekamilika
katika Kristo. 29 [h]Kwa ajili ya jambo hili,
ninajitaabisha, nikijitahidi kwa kadiri ya
nguvu zake ambazo hutenda kazi ndani
yangu kwa uweza mwingi.

2 [i]Nataka mjue jinsi ninavyojitaabisha kwa
ajili yenu na kwa ajili ya wale walioko
Laodikia, na pia kwa ajili ya wote ambao
hawajapata kuniona mimi binafsi. 2 [j]Kusudi
langu ni watiwe moyo na kuunganishwa
katika upendo, ili wapate ule utajiri wa
ufahamu mkamilifu, ili waijue siri ya
Mungu, yaani, Kristo mwenyewe, 3 [k]ambaye
ndani yake kumefichwa hazina zote za
hekima na maarifa. 4 [l]Nawaambia mambo
haya ili mtu yeyote asiwadanganye kwa
maneno ya kuwashawishi. 5 [m]Kwa kuwa
ingawa mimi siko pamoja nanyi kimwili,
lakini niko pamoja nanyi kiroho, nami
nafurahi kuuona utaratibu wenu na jinsi
uthabiti wa imani yenu katika Kristo ulivyo.

*Ukamilifu Wa Maisha Katika Kristo*

6 [n]Hivyo basi, kama vile mlivyompokea
Kristo Yesu kuwa Bwana, endeleeni
kukaa ndani yake, 7 [o]mkiwa na mizizi, na
mmejengwa ndani yake, mkiimarishwa
katika imani kama mlivyofundishwa, na
kufurika kwa wingi wa shukrani.
8 [p]Angalieni mtu yeyote asiwafanye ninyi
mateka kwa elimu batili na madanganyo
matupu yanayotegemea mapokeo ya
wanadamu na mafundisho ya ulimwengu
badala ya Kristo.
9 [q]Maana ukamilifu wote wa Uungu umo
ndani ya Kristo katika umbile la mwili wa
kibinadamu, 10 [r]nanyi mmepewa ukamilifu
ndani ya Kristo, ambaye ndiye mkuu juu ya
kila enzi na kila mamlaka. 11 [s]Katika Kristo
pia mlitahiriwa kwa kutengwa mbali na
asili ya dhambi, si kwa tohara inayofanywa
kwa mikono ya wanadamu, bali kwa ile
tohara iliyofanywa na Kristo, 12 [t]mkiwa

[a]**1:21** Rum 5:10; Efe 2:3
[b]**1:22** Kol 1:20; Rum 5:10; 7:4; 2Kor 4:14; Efe 1:4; 5:27
[c]**1:24** 2Kor 6:10; 1:5; 1Kor 12:27
[d]**1:25** Kol 1:23; 1Kor 3:5; Efe 3:2; Ebr 4:12
[e]**1:26** Rum 16:25
[f]**1:27** Mt 13:11; Rum 2:11, 24; 8:10
[g]**1:28** Kol 3:16; 1Kor 2:6, 7; Mt 5:48; Efe 5:27
[h]**1:29** 1Kor 15:10; 2Kor 11:23; Kol 2:1; Efe 1:19; 3:7
[i]**2:1** Kol 1:29; 4:12; 4:13, 15, 16; Ufu 1:11
[j]**2:2** Efe 6:22; Kol 4:8; Rum 16:25
[k]**2:3** Isa 11:2; Yer 23:5; Rum 11:33; 1Kor 1:24, 30
[l]**2:4** Rum 16:18
[m]**2:5** 1Kor 5:4; 1The 2:17
[n]**2:6** Yn 13:13; Kol 1:10
[o]**2:7** Efe 3:17; 4:22
[p]**2:8** 1Tim 6:20; Kol 2:20; Gal 4:2
[q]**2:9** Yn 1:16
[r]**2:10** Efe 1:22; Mt 28:18
[s]**2:11** Rum 2:29; Flp 3:3; Gal 5:24
[t]**2:12** Mt 28:19; Rum 6:5; Mdo 2:24

mmezikwa pamoja naye katika ubatizo, na
kufufuliwa pamoja naye kwa njia ya imani
yenu katika uweza wa Mungu, aliyemfufua
kutoka kwa wafu.
[13] [a]Mlipokuwa wafu katika dhambi
zenu na kutokutahiriwa katika asili yenu
ya dhambi, Mungu aliwafanya mwe hai
pamoja na Kristo. Alitusamehe dhambi
zetu zote, [14] [b]akiisha kuifuta ile hati yenye
mashtaka yaliyokuwa yanatukabili, pamoja
na maagizo yake. Aliiondoa isiwepo tena,
akiigongomea kwenye msalaba wake.
[15] [c]Mungu akiisha kuzivua enzi na mamlaka,
alizifanya kuwa kitu cha fedheha hadharani
kwa kuziburura kwa ujasiri, akizishinda
katika msalaba wa Kristo.
[16] [d]Kwa hiyo mtu asiwahukumu ninyi
kuhusu vyakula au vinywaji, au kuhusu
kuadhimisha sikukuu za dini, au Sikukuu
za Mwezi Mwandamo au siku ya Sabato.
[17] [e]Hizi zilikuwa kivuli cha mambo ambayo
yangekuja, lakini ile iliyo halisi imo ndani ya
Kristo. [18] [f]Mtu yeyote asiwaondolee thawabu
yenu kwa kusisitiza kunyenyekea kwake na
kuabudu malaika. Mtu kama huyo hudumu
katika maono yake, akijivuna bila sababu
katika mawazo ya kibinadamu. [19] [g]Yeye
amepoteza ushirikiano na Kichwa, ambaye
kutoka kwake mwili wote unalishwa na
kushikamanishwa pamoja kwa viungo na
mishipa, nao hukua kwa ukuaji utokao kwa
Mungu.

*Maonyo Dhidi Ya Walimu Wa Uongo*

[20] Kwa kuwa mlikufa pamoja na Kristo,
mkayaacha yale mafundisho ya msingi ya
ulimwengu huu, kwa nini bado mnaishi
kama ninyi ni wa ulimwengu? Kwa nini
mnajitia chini ya amri: [21] [h]"Msishike!
Msionje! Msiguse!"? [22] [i]Haya yote mwisho
wake ni kuharibika yanapotumiwa, kwa
sababu msingi wake ni katika maagizo
na mafundisho ya wanadamu. [23] [j]Kwa
kweli amri kama hizo huonekana kama
zina hekima, katika namna za ibada
walizojitungia wenyewe, na unyenyekevu
wa uongo na kuutawala mwili kwa ukali,
lakini hayafai kitu katika kuzuia tamaa za
mwili.

*Kanuni Za Kuishi Maisha Matakatifu*

3 [k]Basi, kwa kuwa mmefufuliwa pamoja
na Kristo, yatafuteni yaliyo juu, Kristo
alikoketi mkono wa kuume wa Mungu.
[2] [l]Yafikirini mambo yaliyo juu, wala si
ya duniani. [3] [m]Kwa maana ninyi mlikufa,
nao uhai wenu sasa umefichwa pamoja na
Kristo katika Mungu. [4] [n]Wakati Kristo, aliye
uzima wenu, atakapotokea, ndipo nanyi
mtakapotokea pamoja naye katika utukufu.
[5] [o]Kwa hiyo, ueni kabisa chochote kilicho
ndani yenu cha asili ya kidunia: yaani
uasherati, uchafu, tamaa mbaya, mawazo
mabaya na ulafi, ambayo ndiyo ibada ya
sanamu. [6] [p]Kwa sababu ya mambo haya,
ghadhabu ya Mungu inakuja. [7] [q]Ninyi
pia zamani mlienenda katika mambo
haya mlipoishi maisha hayo. [8] [r]Lakini
sasa yawekeni mbali nanyi mambo
kama haya yote: yaani hasira, ghadhabu,
uovu, masingizio na lugha chafu kutoka
midomoni mwenu. [9] [s]Msiambiane uongo,
kwa maana mmevua kabisa utu wenu wa
kale pamoja na matendo yake, [10] [t]nanyi
mmevaa utu mpya, unaofanywa upya katika
ufahamu sawasawa na mfano wa Muumba

[a]**2:13** Efe 2:15; 2:5; 4:32
[b]**2:14** Efe 2:15; 1Pet 2:24
[c]**2:15** Kol 2:10; Efe 6:12; Mt 12:29; Lk 10:18; Yn 12:31
[d]**2:16** Rum 14:3, 4; Mk 7:19; Rum 14:17; Law 23:2; Rum 14:5
[e]**2:17** Ebr 8:5; 10:1
[f]**2:18** Kol 2:23; 1Kor 9:24; Flp 3:14
[g]**2:19** Efe 1:22; 1Kor 2:8; Gal 4:3, 9, 14, 16
[h]**2:21** 1Tim 4:3
[i]**2:22** 1Kor 6:13; Isa 29:13; Mt 15:9; Tit 1:14
[j]**2:23** Kol 2:18
[k]**3:1** Rum 6:5; Mk 16:19
[l]**3:2** Flp 3:19, 20
[m]**3:3** Rum 6:2; 2Kor 5:14
[n]**3:4** 1Kor 1:7; 1Pet 1:13; 1Yn 3:2; Gal 2:20; 1Kor 1:7; 1Pet 1:13; Yn 3:2
[o]**3:5** Efe 5:3-5; Rum 6:2; Efe 4:22; Gal 5:24; 1Kor 6:18; Efe 5:3; Gal 5:19-21
[p]**3:6** Rum 1:18
[q]**3:7** Efe 2:2
[r]**3:8** Efe 4:22-31
[s]**3:9** Efe 4:22-25
[t]**3:10** Rum 1:22; 2Kor 4:16; Efe 2:10

wake. 11 [a]Hapa hakuna Myunani wala
Myahudi, aliyetahiriwa wala asiyetahiriwa,
asiyestaarabika wala aliyestaarabika,
mtumwa wala mtu huru, bali Kristo ni yote,
na ndani ya wote.
12 [b]Kwa hiyo, kwa kuwa ninyi mmekuwa
wateule wa Mungu, watakatifu wapendwao
sana, jivikeni moyo wa huruma, utu
wema, unyenyekevu, upole na uvumilivu.
13 [c]Vumilianeni na kusameheana mtu
akiwa na lalamiko lolote dhidi ya
mwenzake. Sameheaneni kama vile Bwana
alivyowasamehe ninyi. 14 [d]Zaidi ya maadili
haya yote jivikeni upendo, ambao ndio
unaofunga kila kitu pamoja katika umoja
mkamilifu.
15 [e]Amani ya Kristo na itawale mioyoni
mwenu, kwa kuwa ninyi kama viungo
vya mwili mmoja mmeitiwa amani. Tena
kuweni watu wa shukrani. 16 [f]Neno la
Kristo na likae kwa wingi ndani yenu,
mkifundishana na kuonyana katika hekima
yote, mkimwimbia Mungu zaburi, nyimbo
na tenzi za rohoni, huku mkiwa na shukrani
mioyoni mwenu. 17 [g]Lolote mfanyalo, ikiwa
ni kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote
katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru
Mungu Baba katika yeye.

### *Kanuni Katika Madaraka Ya Nyumbani*

18 Ninyi wake, watiini waume zenu, kama
inavyostahili katika Bwana.
19 [h]Ninyi waume, wapendeni wake zenu,
wala msiwe na uchungu dhidi yao.
20 [i]Enyi watoto, watiini wazazi wenu
katika mambo yote, kwa maana hivi ndivyo
inavyompendeza Bwana.
21 [j]Ninyi akina baba, msiwachokoze
watoto wenu, wasije wakakata tamaa.
22 [k]Ninyi watumwa, watiini mabwana
zenu wa hapa duniani katika mambo
yote. Fanyeni hivyo si wakiwepo tu, wala
si kwa kutafuta upendeleo wao, bali kwa
moyo mnyofu na kumcha Bwana. 23 [l]Lolote
mfanyalo, fanyeni kwa moyo kama watu
wanaomtumikia Bwana, na si wanadamu,
24 [m]kwa kuwa mnajua kwamba mtapokea
urithi wenu kutoka kwa Bwana ukiwa
thawabu yenu. Ni Bwana Yesu Kristo
mnayemtumikia. 25 [n]Yeyote atendaye
mabaya atalipwa kwa ajili ya mabaya yake,
wala hakuna upendeleo.

4 [o]Ninyi mabwana, watendeeni watumwa
wenu yaliyo haki na yanayostahili,
mkitambua ya kwamba ninyi pia mnaye
Bwana mbinguni.

### *Maagizo Zaidi*

2 [p]Dumuni sana katika maombi, mkikesha
katika hayo pamoja na kushukuru. 3 [q]Pia
tuombeeni na sisi ili Mungu atufungulie
mlango wa kunena, ili tupate kuitangaza
siri ya Kristo, ambayo kwa ajili yake pia
mimi nimefungwa. 4 [r]Ombeni ili nipate
kuitangaza Injili kwa udhahiri kama
ipasavyo kunena. 5 [s]Enendeni kwa hekima
mbele yao walio nje, mkiukomboa wakati.
6 [t]Maneno yenu yawe yamejaa neema siku
zote, yanayofaa, ili mjue jinsi iwapasavyo
na inavyofaa kumjibu kila mtu.

### *Salamu Za Mwisho*

7 [u]Tikiko atawaambia habari zangu zote.
Yeye ni ndugu mpendwa, mtendakazi
mwaminifu na mtumishi mwenzangu
katika Bwana. 8 [v]Nimemtuma kwenu kwa
madhumuni haya ili mpate kufahamu

---

[a]**3:11** Rum 10:12; 1Kor 7:19; Gal 3:28; Efe 1:23
[b]**3:12** Flp 2:3; 2Kor 6:6; Gal 5:22, 23; Efe 4:2
[c]**3:13** Efe 4:2, 32; 4:32
[d]**3:14** 1Kor 13:1-13; Efe 4:3
[e]**3:15** Yn 14:27
[f]**3:16** Rum 10:17; Kol 1:28; Efe 5:19
[g]**3:17** Efe 5:20-22
[h]**3:19** Efe 5:25, 28, 33; 1Pet 3:7; Efe 4:31
[i]**3:20** Efe 6:1; 5:24; Tit 2:9
[j]**3:21** Efe 6:4
[k]**3:22** Efe 6:5; 1Tim 6:1; Tit 2:9; 1Pet 2:18
[l]**3:23** Efe 6:6, 7
[m]**3:24** Mdo 20:32
[n]**3:25** Mdo 10:34
[o]**4:1** Law 25:43, 53
[p]**4:2** Lk 18:1; 1The 5:17; Efe 6:18; Flp 4:6
[q]**4:3** Mdo 14:27; Efe 6:19-20; Rum 15:30; 1Kor 16:9
[r]**4:4** Efe 6:20
[s]**4:5** Efe 5:15; Mk 4:11; Efe 5:16
[t]**4:6** Efe 4:29; Mk 9:50; 1Pet 3:15
[u]**4:7** Mdo 20:4; Efe 6:21-22
[v]**4:8** Efe 6:22; 6:21

hali yetu, na pia awatie moyo. 9 [a]Anakuja
pamoja na Onesimo, ndugu yetu mpendwa
na mwaminifu, ambaye ni mmoja wenu.
Watawaambia mambo yote yanayotendeka
hapa kwetu.
10 [b]Aristarko aliye mfungwa pamoja
nami anawasalimu, vivyo hivyo Marko,
binamu yake Barnaba. (Mmeshapata
maagizo yanayomhusu; akija kwenu,
mpokeeni.) 11 [c]Yesu, yeye aitwaye Yusto,
pia anawasalimu. Hawa peke yao ndio
Wayahudi miongoni mwa watendakazi
wenzangu kwa ajili ya Ufalme wa Mungu,
nao wamekuwa faraja kwangu. 12 [d]Epafra,
ambaye ni mmoja wenu na mtumishi
wa Kristo Yesu, anawasalimu. Yeye siku
zote anawaombea kwa bidii kwamba
msimame imara katika mapenzi yote ya
Mungu, mkiwa wakamilifu na thabiti.
13 [e]Ninashuhudia kumhusu kwamba
anafanya kazi kwa bidii kwa ajili yenu, na
kwa ajili ya ndugu wa Laodikia na wale wa
Hierapoli. 14 [f]Rafiki yetu mpenzi Luka yule
tabibu, pamoja na Dema, wanawasalimu.
15 [g]Wasalimuni ndugu wote wa Laodikia, na
pia Nimfa, pamoja na kanisa linalokutana
katika nyumba yake.

16 [h]Baada ya barua hii kusomwa kwenu, hakikisheni kwamba inasomwa pia katika kanisa la Walaodikia. Nanyi pia msome barua inayotoka Laodikia.

17 [i]Mwambieni Arkipo hivi: "Hakikisha kuwa unakamilisha ile huduma uliyopokea katika Bwana."

18 [j]Mimi, Paulo, naandika salamu hizi kwa mkono wangu mwenyewe. Kumbukeni minyororo yangu. Neema iwe nanyi. Amen.

---

[a]**4:9** Flp 1:10; Flm 10; Kol 4:12
[b]**4:10** Mdo 19:21; 4:36
[c]**4:11** Flp 2:25
[d]**4:12** Kol 1:7; Flp 1:23; Rum 15:30; 1Kor 2:6
[e]**4:13** Kol 2:1
[f]**4:14** 2Tim 4:11; Flp 1:24; 2Tim 4:10
[g]**4:15** Rum 16:5
[h]**4:16** 2The 3:14
[i]**4:17** Flp 1:2; 2Tim 4:5
[j]**4:18** 1Kor 16:21; Ebr 13:3

# 1 WATHESALONIKE

*Salamu*

1 [a]Paulo, Silvano[b] na Timotheo:
Kwa kanisa la Wathesalonike, ninyi
mlio ndani ya Mungu Baba yetu na ndani
ya Bwana Yesu Kristo:
Neema iwe kwenu na amani.

*Shukrani Kwa Ajili Ya Imani Ya Wathesalonike*

2 [c]Siku zote tunamshukuru Mungu kwa
ajili yenu ninyi nyote, tukiwataja kwenye
maombi yetu daima. 3 [d]Tunaikumbuka
daima kazi yenu ya imani mbele za Mungu
aliye Baba yetu, taabu yenu katika upendo
na saburi yenu ya tumaini katika Bwana
wetu Yesu Kristo.
4 [e]Ndugu zetu mpendwao na Mungu,
kwa kuwa tunajua kwamba Mungu
amewachagua, 5 [f]kwa sababu ujumbe
wetu wa Injili haukuja kwenu kwa maneno
matupu bali pia ulidhihirishwa katika
nguvu na katika Roho Mtakatifu, tena
ukiwa na uthibitisho kamili, kama vile ninyi
wenyewe mnavyojua jinsi tulivyoenenda
katikati yenu kwa ajili yenu. 6 [g]Nanyi
mkawa wafuasi wetu na wa Bwana, ingawa
mlipata mateso mengi, mlilipokea lile Neno
kwa furaha katika Roho Mtakatifu. 7 [h]Hivyo
ninyi mkawa kielelezo kwa waumini wote
katika Makedonia na Akaya. 8 [i]Kwa maana
kutoka kwenu neno la Bwana limesikika,
si katika Makedonia na Akaya tu, bali pia
imani yenu katika Mungu imejulikana
kila mahali kiasi kwamba hatuna haja ya
kusema lolote kwa habari yake. 9 [j]Kwa
maana watu wa maeneo hayo wenyewe
wanaeleza jinsi mlivyotupokea na jinsi
mlivyomgeukia Mungu mkaacha sanamu,
ili kumtumikia Mungu aliye hai na wa
kweli 10 [k]na ili kumngojea Mwanawe kutoka
mbinguni, ambaye Mungu alimfufua kutoka
kwa wafu: yaani, Yesu, yeye aliyetuokoa
kutoka ghadhabu inayokuja.

*Huduma Ya Paulo Huko Thesalonike*

2 [l]Ndugu zangu, kwa kuwa ninyi wenyewe
mnajua ya kwamba kuja kwetu kwenu
hakukuwa bure, 2 [m]kama vile mjuavyo,
tulikuwa tumeteswa na kutukanwa huko
Filipi, lakini hata hivyo, kwa msaada
wa Mungu wetu, tulikuwa na ujasiri
wa kuwaambia Injili ya Mungu ingawa
kulikuwa na upinzani mkubwa. 3 [n]Kwa
maana himizo letu halikutokana na hila
wala nia mbaya au udanganyifu. 4 [o]Kinyume
chake, tulinena kama watu tuliokubaliwa na
Mungu tukakabidhiwa Injili. Sisi hatujaribu
kuwapendeza wanadamu bali kumpendeza
Mungu, yeye ayachunguzaye mawazo
ya ndani sana ya mioyo yetu. 5 [p]Kama
mjuavyo, hatukuja kwenu kwa maneno ya
kujipendekeza au maneno yasiyo ya kweli
ili kuficha tamaa mbaya: Mungu ndiye
shahidi yetu. 6 [q]Wala hatukuwa tunatafuta
sifa kutoka kwa wanadamu, wala kutoka
kwenu au kwa mtu mwingine awaye yote.
Kama mitume wa Kristo tungaliweza kuwa
mzigo kwenu, 7 [r]lakini tulikuwa wapole
katikati yenu, kama mama anayewatunza
watoto wake wadogo. 8 [s]Tuliwapenda sana
kiasi kwamba tulifurahia kushirikiana
nanyi, si Injili ya Mungu tu, bali hata maisha
yetu, kwa sababu mlikuwa wa thamani mno

---

[a]**1:1** Mdo 16:1; 17:1; Rum 1:7
[b]1 Yaani Sila.
[c]**1:2** Rum 1:8; 2The 1:11; Efe 1:16; Flm 4
[d]**1:3** 2The 1:11; 1The 2:13; Yn 6:29; Gal 5:6; 1The 3:6; Yak 2:17; Rum 16:6
[e]**1:4** Kol 3:12; 2The 2:13
[f]**1:5** 2The 2:14; Mk 16:20; 1Kor 6:6; Kol 2:2
[g]**1:6** 1Kor 4:16; Mdo 17:5-10; 13:52
[h]**1:7** 1The 4:10; Flp 3:7; 1Pet 5:3; 1Tim 4:12
[i]**1:8** Rum 1:8; 10:18
[j]**1:9** 1Kor 12:2; Gal 4:8
[k]**1:10** Mdo 2:24; Rum 5:9
[l]**2:1** 1The 1:5-9
[m]**2:2** Mdo 16:22; Flp 1:30
[n]**2:3** 2Kor 2:17
[o]**2:4** Gal 2:7; 1:10
[p]**2:5** Mdo 20:33; Rum 1:9
[q]**2:6** 1Kor 9:1-2
[r]**2:7** 1The 2:11; 1Kor 2:3; 9:22; 2Kor 1:4; 7:6, 7
[s]**2:8** 2Kor 12:15; 1Yn 3:16

kwetu. 9 [a]Ndugu zetu, mnakumbuka juhudi
yetu na taabu yetu. Tulifanya kazi usiku
na mchana, ili tusimlemee mtu yeyote wa
kwenu wakati tulipokuwa tunawahubiria
Injili ya Mungu.
10 [b]Ninyi wenyewe ni mashahidi na
Mungu pia, jinsi tulivyokuwa watakatifu,
wenye haki na wasio na lawama miongoni
mwenu ninyi mlioamini. 11 [c]Maana mnajua
kwamba tuliwatendea kila mmoja wenu
kama vile baba awatendeavyo watoto
wake. 12 [d]Tuliwatia moyo, tuliwafariji na
kuwahimiza kuishi maisha yampendezayo
Mungu, anayewaita katika Ufalme na
utukufu wake.
13 [e]Nasi pia tunamshukuru Mungu
bila kukoma kwa sababu mlipolipokea
neno la Mungu mlilosikia kutoka kwetu,
hamkulipokea kama neno la wanadamu,
bali mlilipokea kama lilivyo hasa, neno la
Mungu, litendalo kazi ndani yenu ninyi
mnaoamini. 14 [f]Kwa maana ninyi ndugu
zetu, mlifanyika wafuasi wa makanisa
ya Mungu yaliyoko ndani ya Kristo Yesu
katika Uyahudi. Mlipata mateso yale
yale kutoka kwa watu wenu wenyewe
kama vile makanisa hayo yalivyoteswa
na Wayahudi, 15 [g]wale waliomuua Bwana
Yesu na manabii, nasi wakatufukuza pia.
Watu hao walimchukiza Mungu na tena
ni adui wa watu wote, 16 [h]wakijitahidi
kutuzuia tusizungumze na watu wa Mataifa
ili kwamba wapate kuokolewa. Kwa njia
hii wanazidi kujilundikia dhambi zao hadi
kikomo. Lakini hatimaye ghadhabu ya
Mungu imewafikia.

*Paulo Atamani Kuwaona Wathesalonike*

17 [i]Lakini ndugu zetu, tulipotenganishwa
nanyi kwa kitambo kidogo (ingawa
kutengana huko kulikuwa kwa mwili tu,
si kwa moyo), tulizidi kuwa na shauku
kubwa kuwaona uso kwa uso. 18 [j]Maana
tulitaka kuja kwenu, hasa mimi Paulo,
nilitaka kuja tena na tena, lakini Shetani
akatuzuia. 19 [k]Kwa maana tumaini letu ni
nini, au furaha yetu au taji yetu ya kujisifia
mbele za Bwana Yesu Kristo wakati wa kuja
kwake? Je, si ni ninyi? 20 [l]Naam, ninyi ndio
fahari yetu na furaha yetu.

*Timotheo Atumwa Kwenda Thesalonike*

3 [m]Kwa hivyo tulipokuwa hatuwezi
kuvumilia zaidi, tuliamua tubaki Athene
peke yetu. 2 [n]Tukamtuma Timotheo ambaye
ni ndugu yetu na mtumishi mwenzetu wa
Mungu katika kuieneza Injili ya Kristo, aje
kuwaimarisha na kuwatia moyo katika
imani yenu, 3 [o]ili mtu yeyote asifadhaishwe
na mateso haya. Mnajua vyema kwamba
tumewekewa hayo mateso. 4 [p]Kwa kweli,
tulipokuwa pamoja nanyi tuliwaambia
mara kwa mara kwamba tutateswa na
imekuwa hivyo kama mjuavyo. 5 [q]Kwa
sababu hii nilipokuwa siwezi kuvumilia
zaidi, nilimtuma mtu ili nipate habari za
imani yenu. Niliogopa kwamba kwa njia
fulani yule mjaribu asiwe amewajaribu,
nasi tukawa tumejitaabisha bure.

*Taarifa Ya Timotheo Ya Kutia Moyo*

6 [r]Lakini sasa Timotheo ndiyo tu amerejea
kwetu kutoka kwenu na ameleta habari
njema kuhusu imani yenu na upendo
wenu. Ametuambia kwamba siku zote
mnatukumbuka kwa wema na kwamba mna
shauku ya kutuona kama vile sisi tulivyo
na shauku ya kuwaona ninyi. 7 Kwa hiyo,
ndugu zetu, katika dhiki na mateso yetu
yote tumefarijika kwa sababu ya imani
yenu. 8 [s]Sasa kwa kuwa hakika tunaishi,

[a]**2:9** Mdo 18:3; 2Kor 11:9; 2The 3:8
[b]**2:10** 2Kor 1:12
[c]**2:11** 1Kor 4:14
[d]**2:12** Efe 4:1
[e]**2:13** Ebr 4:12
[f]**2:14** Gal 1:22; Mdo 17:5; 2The 1:4
[g]**2:15** Mdo 2:23; Mt 5:12
[h]**2:16** Mdo 13:45-50; Mt 23:32
[i]**2:17** 1Kor 5:3; Kol 2:5; 1The 3:10
[j]**2:18** Mt 4:10; Rum 1:13; 15:22
[k]**2:19** Flp 4:1; 2Kor 1:14; Mt 16:27; 1The 3:13
[l]**2:20** 2Kor 1:14
[m]**3:1** Mdo 17:15; 1The 3:5; Mdo 17:14
[n]**3:2** Mdo 16:1; 1Kor 3:9; 2Kor 2:12
[o]**3:3** Mdo 9:16; 14:22
[p]**3:4** 1The 2:14; Mdo 14:22
[q]**3:5** Mt 4:3; Gal 2:2; Flp 2:16
[r]**3:6** Mdo 18:5
[s]**3:8** 1Kor 16:13

kwa kuwa ninyi mmesimama imara katika
Bwana. 9 [a]Je, tutawezaje kumshukuru
Mungu kiasi cha kutosha kwa ajili yenu,
kutokana na furaha tuliyo nayo mbele za
Mungu wetu kwa sababu yenu? 10 [b]Usiku
na mchana tunaomba kwa bidii ili tupate
kuwaona tena na kujaza kile kilichopungua
katika imani yenu.

11 [c]Basi Mungu wetu na Baba yetu
mwenyewe na Bwana wetu Yesu atengeneze
njia ya sisi kuja kwenu. 12 [d]Bwana na
auongeze upendo wenu na kuuzidisha
kati yenu na kwa wengine wote, kama
vile tulivyo na upendo mwingi kwenu.
13 Tunamwomba Mungu aimarishe mioyo
yenu ili msiwe na lawama katika utakatifu
mbele za Mungu wetu aliye Baba yetu
wakati wa kuja kwake Bwana Yesu pamoja
na watakatifu wote.

*Maisha Yanayompendeza Mungu*

4 [e]Hatimaye, ndugu, tuliwaomba na
kuwasihi katika Bwana Yesu kwamba,
kama mlivyojifunza kutoka kwetu jinsi
iwapasavyo kuishi ili kumpendeza Mungu,
kama vile mnavyoishi, imewapasa mzidi
sana kufanya hivyo. 2 Kwa kuwa mnajua
ni maagizo gani tuliyowapa kwa mamlaka
ya Bwana Yesu.

3 [f]Mapenzi ya Mungu ni kwamba ninyi
mtakaswe, ili kwamba mjiepushe na zinaa,
4 [g]ili kwamba kila mmoja wenu ajifunze
kuutawala mwili wake mwenyewe katika
utakatifu na heshima, 5 [h]si kwa tamaa
mbaya kama watu wa Mataifa wasiomjua
Mungu. 6 [i]Katika jambo hili mtu asimkosee
ndugu yake wala kumlaghai. Kwa kuwa
Bwana ni mlipiza kisasi katika mambo haya
yote, kama vile tulivyokwisha kuwaambia
mapema na kuwaonya vikali. 7 [j]Kwa maana
Mungu hakutuitia uchafu, bali utakatifu.
8 [k]Kwa hiyo, mtu yeyote anayekataa
mafundisho haya hamkatai mwanadamu,
bali anamkataa Mungu anayewapa ninyi
Roho wake Mtakatifu.

9 [l]Sasa kuhusu upendo wa ndugu
hamna haja mtu yeyote kuwaandikia, kwa
maana ninyi wenyewe mmefundishwa na
Mungu kupendana. 10 [m]Nanyi kwa kweli
mnawapenda ndugu wote katika Makedonia
nzima. Lakini ndugu, tunawasihi mzidi sana
kuwapenda.

11 [n]Jitahidini kuishi maisha ya utulivu,
kila mtu akijishughulisha na mambo
yake mwenyewe na kufanya kazi kwa
mikono yake, kama vile tulivyowaagiza,
12 [o]ili maisha yenu ya kila siku yajipatie
heshima kutoka kwa watu walio nje, ili
msimtegemee mtu yeyote.

*Kuja Kwake Bwana*

13 [p]Lakini ndugu, hatutaki mkose kujua
kuhusu wale waliolala mauti, ili msihuzunike
kama watu wengine wasiokuwa na
tumaini. 14 [q]Kwa kuwa tunaamini kwamba
Yesu alikufa na kufufuka, na kwa hivyo,
Mungu kwa njia ya Yesu atawafufua pamoja
naye wale waliolala mautini ndani yake.
15 [r]Kulingana na neno la Bwana mwenyewe,
tunawaambia kwamba sisi ambao bado
tuko hai, tuliobaki hadi kuja kwake Bwana,
hakika hatutawatangulia waliolala mauti.
16 [s]Kwa maana Bwana mwenyewe atashuka
kutoka mbinguni, akitoa amri kwa sauti
kuu, pamoja na sauti ya malaika mkuu,
na sauti ya tarumbeta ya Mungu. Nao
waliokufa wakiwa katika Kristo watafufuka
kwanza. 17 [t]Baada ya hilo sisi tulio hai,
tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika

[a]**3:9** 1The 1:2; 2:19, 20
[b]**3:10** 2Tim 1:3; 1The 2:17
[c]**3:11** 1The 3:13; Flp 4:20
[d]**3:12** 1Kor 1:8; 1The 2:19
[e]**4:1** 2Kor 13:11; 5:9
[f]**4:3** 1Kor 6:18
[g]**4:4** 1Kor 7:2-9
[h]**4:5** Rum 1:26; Efe 4:17
[i]**4:6** 1Kor 6:8; Ebr 13:4
[j]**4:7** Law 11:44; 1Pet 1:15
[k]**4:8** Rum 5:5; Gal 4:6
[l]**4:9** Rum 12:10; Yn 13:34; 1The 5:1
[m]**4:10** 1The 1:7; 3:12
[n]**4:11** Efe 4:28; 2The 3:10-12
[o]**4:12** Mk 4:11
[p]**4:13** Efe 2:12
[q]**4:14** 1Kor 15:18
[r]**4:15** 1Kor 15:52
[s]**4:16** Mt 24:31; 1Kor 15:23; 2The 2:1
[t]**4:17** Mdo 1:9; Ufu 11:12; 1Kor 15:52; Yn 12:26

mawingu ili kumlaki Bwana hewani, hivyo
tutakuwa pamoja na Bwana milele. 18 Kwa
hiyo farijianeni kwa maneno haya.

### *Kuweni Tayari Kwa Siku Ya Bwana*

5 [a]Basi, ndugu, kwa habari ya nyakati na
majira hatuna haja ya kuwaandikia,
2 [b]kwa kuwa mnajua vyema kwamba siku
ya Bwana itakuja kama mwizi ajapo usiku.
3 [c]Wakati watu wanaposema, "Kuna amani
na salama," maangamizi huwajia ghafula,
kama vile utungu umjiavyo mwanamke
mwenye mimba; nao hakika hawatatoroka.
4 [d]Bali ninyi, ndugu, hampo gizani hata
siku ile iwakute ghafula kama mwizi.
5 [e]Ninyi nyote ni wana wa nuru na wana
wa mchana. Sisi si wana wa giza wala
wa usiku. 6 [f]Kwa hiyo basi, tusilale kama
watu wengine walalavyo, bali tukeshe na
kuwa na kiasi. 7 [g]Kwa kuwa wote walalao
hulala usiku na wale walewao hulewa
usiku. 8 [h]Lakini kwa kuwa sisi ni wana wa
mchana, basi tuwe na kiasi, tukijivika imani
na upendo kama dirii kifuani na tumaini
letu la wokovu kama chapeo. 9 [i]Kwa maana
Mungu hakutuita ili tupate ghadhabu bali
tupate wokovu kwa njia ya Bwana wetu
Yesu Kristo. 10 [j]Yeye alikufa kwa ajili yetu ili
hata kama tuko macho au tumelala, tupate
kuishi pamoja naye. 11 [k]Kwa hiyo farijianeni
na kujengana, kama vile mnavyofanya sasa.

### *Maagizo Ya Mwisho, Salamu Na Kuwatakia Heri*

12 [l]Sasa tunawaomba, ndugu,
waheshimuni wale wanaofanya kazi kwa
bidii miongoni mwenu, wale ambao wana
mamlaka juu yenu katika Bwana na ambao
wanawaonya. 13 [m]Waheshimuni sana katika
upendo kwa ajili ya kazi zao. Ishini kwa
amani ninyi kwa ninyi. 14 [n]Nasi twawasihi,
ndugu, waonyeni walio wavivu, watieni
moyo waoga, wasaidieni wanyonge na
kuwavumilia watu wote. 15 [o]Angalieni
kuwa mtu asimlipe mwenzake maovu kwa
maovu, bali siku zote tafuteni kutendeana
mema ninyi kwa ninyi na kwa watu wote.
16 [p]Furahini siku zote; 17 [q]ombeni bila
kukoma; 18 [r]shukuruni kwa kila jambo, kwa
maana haya ndiyo mapenzi ya Mungu kwa
ajili yenu katika Kristo Yesu.
19 [s]Msiuzime moto wa Roho Mtakatifu;
20 [t]msiyadharau maneno ya unabii.
21 [u]Jaribuni kila kitu. Yashikeni yaliyo
mema. 22 [v]Jiepusheni na uovu wa kila
namna.
23 [w]Mungu mwenyewe, Mungu wa amani,
awatakase ninyi kabisa. Nanyi mhifadhiwe
roho zenu, nafsi zenu na miili yenu, bila
kuwa na lawama katika Bwana wetu Yesu
Kristo. 24 [x]Yeye aliyewaita ni mwaminifu
naye atafanya hayo.
25 [y]Ndugu, tuombeeni. 26 Wasalimuni
ndugu wote kwa busu takatifu.
27 Nawaagizeni mbele za Bwana mhakikishe
kuwa ndugu wote wanasomewa barua hii.
28 Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo iwe
nanyi. Amen.

---

[a]**5:1** Mdo 1:7; 1The 4:9
[b]**5:2** 1Kor 1:8; 2Pet 3:10
[c]**5:3** Yer 6:14; Yn 16:21, 22; Mt 24:39; Lk 21:34, 35
[d]**5:4** Mdo 26:18; 1Yn 2:8
[e]**5:5** Rum 13:12; Efe 5:9
[f]**5:6** Rum 13:11
[g]**5:7** Lk 21:34, 36; Rum 13:13; 1Kor 15:34
[h]**5:8** Isa 59:17; Efe 6:14, 16, 17
[i]**5:9** 2The 2:13-14
[j]**5:10** 2Kor 5:15
[k]**5:11** 1The 4:18
[l]**5:12** 1Tim 5:17; Ebr 13:17
[m]**5:13** Mk 9:50; 2The 3:6-11; Rum 14:1
[n]**5:14** 2The 3:11, 12; Ebr 12:12; Rum 4:1; 15:1
[o]**5:15** 1Pet 3:9; Gal 6:10; Efe 4:32
[p]**5:16** 2Kor 6:10; Flp 4:4
[q]**5:17** Lk 18:1; 21:36; Rum 12:12; Efe 6:18; Kol 4:12
[r]**5:18** Efe 5:20; Kol 3:17
[s]**5:19** Efe 4:30
[t]**5:20** 1Kor 14:1-40
[u]**5:21** 1Kor 14:29; 1Yn 4:1
[v]**5:22** 1The 4:12
[w]**5:23** Rum 15:33; Ebr 4:12; 1The 3:13; 2:19
[x]**5:24** Rum 8:28; 1Kor 1:9; Hes 23:19; Flp 1:6
[y]**5:25** Kol 4:3; 2The 3:1; Ebr 13:18; Efe 6:9

# 2 WATHESALONIKE

1 [a]Paulo, Silvano[b] na Timotheo:
Kwa kanisa la Wathesalonike mlio
katika Mungu Baba yetu na Bwana Yesu
Kristo:
2 [c]Neema na amani itokayo kwa Mungu
Baba na Bwana Yesu Kristo iwe nanyi.

### *Shukrani Na Maombi*

3 [d]Ndugu, imetubidi kumshukuru Mungu
kwa ajili yenu siku zote, kama ulivyo wajibu
wetu, kwa sababu imani yenu inakua zaidi
na zaidi na upendo wa kila mmoja wenu alio
nao kwa mwenzake unazidi kuongezeka.
4 [e]Ndiyo sababu miongoni mwa makanisa
ya Mungu, tunajivuna kuhusu saburi yenu
na imani mliyo nayo katika mateso yote na
dhiki mnazostahimili.
5 [f]Haya yote ni uthibitisho kwamba
hukumu ya Mungu ni ya haki, na kwa sababu
hiyo ninyi mtahesabiwa kwamba mnastahili
kuwa wa Ufalme wa Mungu, mnaoteswa
kwa ajili wake. 6 [g]Mungu ni mwenye haki:
yeye atawalipa mateso wale wawatesao
ninyi 7 [h]na kuwapa ninyi mnaoteseka
raha pamoja na sisi, wakati Bwana Yesu
atakapodhihirishwa kutoka mbinguni
katika mwali wa moto pamoja na malaika
wake wenye nguvu. 8 [i]Atawaadhibu wale
wasiomjua Mungu na ambao hawakuitii
Injili ya Bwana wetu Yesu. 9 [j]Wataadhibiwa
kwa uangamivu wa milele na kutengwa na
uso wa Bwana na utukufu wa uweza wake,
10 [k]siku hiyo atakapokuja kutukuzwa katika
watakatifu wake na kustaajabiwa miongoni
mwa wote walioamini. Ninyi pia mtakuwa
miongoni mwa hawa kwa sababu mliamini
ushuhuda wetu kwenu.
11 [l]Kwa sababu hii, tunawaombea ninyi
bila kukoma, ili Mungu apate kuwahesabu
kuwa mnastahili wito wake na kwamba kwa
uwezo wake apate kutimiza kila kusudi lenu
jema na kila tendo linaloongozwa na imani
yenu. 12 [m]Tunaomba hivi ili Jina la Bwana
wetu Yesu lipate kutukuzwa ndani yenu,
nanyi ndani yake, kulingana na neema ya
Mungu wetu na Bwana Yesu Kristo.

### *Yule Mtu Wa Kuasi*

2 [n]Ndugu, kuhusu kuja kwake Bwana wetu
Yesu Kristo na kukusanyika kwetu pamoja
mbele zake, tunawasihi, 2 [o]msiyumbishwe
kwa urahisi wala msitiwe wasiwasi na roho
wala neno au barua inayosemekana kuwa
imetoka kwetu, isemayo kwamba siku ya
Bwana imekwisha kuwako. 3 [p]Mtu yeyote
na asiwadanganye kwa namna yoyote
kwa maana siku ile haitakuja mpaka uasi
utokee kwanza, na yule mtu wa kuasi
adhihirishwe, yule ambaye amehukumiwa
kuangamizwa kabisa. 4 [q]Yeye atapingana
na kujitukuza juu ya kila kitu kiitwacho
Mungu au kinachoabudiwa, ili kujiweka
juu katika Hekalu la Mungu, akijitangaza
mwenyewe kuwa ndiye Mungu.
5 [r]Je, hamkumbuki ya kwamba
nilipokuwa pamoja nanyi niliwaambia
mambo haya? 6 [s]Nanyi sasa mnajua
kinachomzuia, ili apate kudhihirishwa
wakati wake utakapowadia. 7 [t]Maana ile
nguvu ya siri ya uasi tayari inatenda kazi,
lakini yule anayeizuia ataendelea kufanya
hivyo mpaka atakapoondolewa. 8 [u]Hapo
ndipo yule mwasi atafunuliwa, ambaye
Bwana Yesu atamteketeza kwa pumzi ya

---

[a]**1:1** Mdo 16:1; 1The 1:1
[b]1 Yaani Sila.
[c]**1:2** Rum 1:7; 1Kor 1:3
[d]**1:3** 1The 3:12; 1:2, 3; 2The 2:13
[e]**1:4** 2Kor 7:14; 1The 1:3; 1:6
[f]**1:5** Flp 1:28
[g]**1:6** Rum 12:19; Ufu 6:10
[h]**1:7** 1The 4:16; Yud 14
[i]**1:8** Gal 4:8; Rum 2:8
[j]**1:9** 1The 5:3; 2Pet 3:7; 2The 2:8
[k]**1:10** 1Kor 3:13; Yn 17:10; 1Kor 1:6
[l]**1:11** 1The 1:3; 2The 1:5
[m]**1:12** Flp 2:9, 11; 1Pet 1:7; 4:14
[n]**2:1** Mk 13:27; 1The 4:15-17
[o]**2:2** 2The 3:17; 1Kor 1:8
[p]**2:3** Mk 13:5; Dan 8:25; Ufu 13:5, 6
[q]**2:4** 1Kor 8:5; Isa 14:13, 14; Eze 28:2
[r]**2:5** 1The 3:4
[s]**2:6** 2The 2:7
[t]**2:7** 2The 2:6
[u]**2:8** Isa 11:4; Ufu 2:16

kinywa chake na kumwangamiza kabisa
kwa utukufu wa kuja kwake. 9 [a]Kuja kwa
yule mwasi kutaonekana kana kwamba
ni kutenda kazi kwake Shetani ambaye
hutumia nguvu zote, ishara, maajabu ya
uongo, 10 [b]na kila aina ya uovu kwa wale
wanaoangamia kwa sababu walikataa
kuipenda kweli wapate kuokolewa. 11 [c]Kwa
sababu hii, Mungu ameruhusu watawaliwe
na nguvu ya udanganyifu, ili waendelee
kuamini uongo, 12 [d]na wahukumiwe wote
ambao hawakuiamini ile kweli, bali
wamefurahia uovu.

*Simameni Imara*

13 [e]Lakini imetupasa sisi kumshukuru
Mungu daima kwa ajili yenu, ndugu
mpendwao na Bwana, kwa sababu Mungu
aliwachagua ninyi tangu mwanzo ili
mwokolewe kwa kutakaswa na Roho kwa
kuiamini kweli. 14 [f]Kwa kusudi hili Mungu
aliwaita kwa njia ya kuhubiri kwetu Injili,
ili mpate kushiriki katika utukufu wa
Bwana Yesu Kristo. 15 [g]Hivyo basi, ndugu
wapendwa, simameni imara na myashike
sana yale mafundisho tuliyowapa ikiwa ni
kwa maneno ya kinywa au kwa barua.

16 [h]Bwana wetu Yesu Kristo mwenyewe
na Mungu Baba yetu, aliyetupenda na kwa
neema yake akatupatia faraja ya milele na
tumaini jema, 17 [i]awafariji mioyo yenu na
kuwaimarisha katika kila neno na tendo
jema.

*Hitaji La Maombi*

3 [j]Hatimaye, ndugu, tuombeeni ili Neno
la Bwana lipate kuenea kwa haraka
na kuheshimiwa kila mahali, kama vile
ilivyokuwa kwenu. 2 [k]Ombeni pia ili tupate
kuokolewa kutokana na watu waovu na
wabaya, kwa maana si wote wanaoamini.
3 [l]Lakini Bwana ni mwaminifu, naye
atawaimarisha ninyi na kuwalinda kutokana
na yule mwovu. 4 [m]Nasi tuna tumaini katika
Bwana ya kuwa mnafanya na mtaendelea
kufanya yale tuliyowaagiza. 5 [n]Bwana
aiongoze mioyo yenu katika upendo wa
Mungu na katika saburi ya Kristo.

*Onyo Dhidi Ya Uvivu*

6 [o]Ndugu, tunawaagiza katika Jina
la Bwana Yesu Kristo, jitengeni na kila
ndugu ambaye ni mvivu na ambaye haishi
kufuatana na maagizo tuliyowapa. 7 [p]Maana
ninyi wenyewe mnajua jinsi iwapasavyo
kufuata mfano wetu. Sisi hatukuwa wavivu
tulipokuwa pamoja nanyi, 8 [q]wala hatukula
chakula cha mtu yeyote pasipo kukilipia.
Badala yake tulifanya kazi kwa bidii usiku
na mchana, ili tusimlemee mtu yeyote
miongoni mwenu. 9 [r]Tulifanya hivi, si kwa
sababu hatukuwa na haki ya kupata msaada
kama huo, bali ndio sisi wenyewe tuwe
kielelezo. 10 [s]Kwa maana hata tulipokuwa
pamoja nanyi, tuliwapa amri kwamba: "Mtu
yeyote asiyetaka kufanya kazi, hata kula
asile."

11 [t]Kwa kuwa tunasikia kwamba baadhi
ya watu miongoni mwenu ni wavivu.
Hawafanyi kazi bali hujishughulisha na
mambo ya wengine. 12 [u]Basi watu kama hao
tunawaagiza na kuwahimiza katika Bwana
Yesu Kristo, kwamba wafanye kazi kwa
utulivu kwa ajili ya chakula chao wenyewe.
13 [v]Kwa upande wenu, ndugu, ninyi kamwe
msichoke katika kutenda mema.

14 [w]Ikiwa mtu yeyote hayatii maagizo

---

[a]**2:9** Mt 24:24; Ufu 13:13
[b]**2:10** 1Kor 1:18
[c]**2:11** Rum 1:28
[d]**2:12** Rum 1:32
[e]**2:13** Efe 1:4; 1The 5:9; 1Pet 1:2
[f]**2:14** Rum 8:28; 11:29; 1The 1:5
[g]**2:15** 1Kor 16:13; 11:2
[h]**2:16** Yn 3:16
[i]**2:17** 1The 3:2; 2The 3:3
[j]**3:1** 1The 4:1; 5:25; 1:8
[k]**3:2** Rum 15:31
[l]**3:3** 1Kor 1:9; Mt 5:37
[m]**3:4** 2Kor 2:3
[n]**3:5** 1Nya 29:18
[o]**3:6** 1Kor 5:4; Rum 16:17; 1Kor 11:2
[p]**3:7** 1Kor 4:16
[q]**3:8** Mdo 18:3; Efe 4:28
[r]**3:9** 1Kor 9:4-14; 4:16
[s]**3:10** 1The 3:4; 4:11
[t]**3:11** 1Tim 5:13
[u]**3:12** 1The 4:1; 4:11; Efe 4:28
[v]**3:13** Gal 6:9
[w]**3:14** Rum 16:17

yetu yaliyoko katika barua hii, mwangalieni
sana mtu huyo. Msishirikiane naye, ili apate
kuona aibu. 15 [a]Lakini msimhesabu kuwa
adui, bali mwonyeni kama ndugu.

*Salamu Za Mwisho*

16 [b]Basi, Bwana wa amani mwenyewe
awapeni amani nyakati zote na kwa kila
njia. Bwana awe nanyi nyote.
17 [c]Mimi, Paulo, ninaandika salamu hizi
kwa mkono wangu mwenyewe. Hii ndio
alama ya utambulisho katika barua zangu
zote. Hivi ndivyo niandikavyo.
18 [d]Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo iwe
nanyi nyote. Amen.

[a]**3:15** Gal 6:1
[b]**3:16** Rum 15:33; Rut 2:4
[c]**3:17** 1Kor 16:21
[d]**3:18** Rum 16:20

# 1 TIMOTHEO

1 [a]Paulo, mtume wa Kristo Yesu kwa amri ya Mungu Mwokozi wetu na ya Kristo Yesu tumaini letu.

2 [b]Kwa Timotheo, mwanangu halisi katika imani:

Neema, rehema na amani itokayo kwa Mungu Baba na kwa Kristo Yesu Bwana wetu.

*Maonyo Dhidi Ya Walimu Wa Uongo*

3 [c]Kama nilivyokusihi wakati nilipokwenda Makedonia, endelea kubaki Efeso, ili kwamba upate kuwaagiza watu wasiendelee kufundisha mafundisho ya uongo 4 [d]wala wasitoe muda wao kwa hadithi za kubuniwa na orodha za majina ya vizazi visivyo na mwisho, ambazo huchochea mabishano badala ya mpango wa Mungu utokanao na imani. 5 [e]Kusudi la maagizo haya ni upendo utokao katika moyo safi, dhamiri njema na imani ya kweli. 6 [f]Watu wengine wamepotoka kutoka haya na kugeukia majadiliano yasiyo na maana kwa kuwa, 7 [g]wanataka kuwa walimu wa sheria, lakini hawajui mambo yale wanayosema wala hayo wanayoyatumainia kwa uthabiti.

8 [h]Tunajua kwamba sheria ni njema ikiwa inatumika kwa halali kama ilivyokusudiwa. 9 [i]Lakini tunajua ya kuwa sheria si kwa ajili ya wenye haki, bali kwa ajili ya wavunja sheria na waasi, kwa ajili ya wasiomcha Mungu na wenye dhambi, wasio watakatifu na wanaokufuru; kwa wale wawauao baba zao au mama zao, kwa wauaji, 10 [j]kwa wazinzi na wahanithi, kwa wale wauzao watu, na kwa waongo na waapao kwa uongo, na kwa chochote kingine kilicho kinyume na mafundisho ya kweli, 11 [k]ambayo yanakubaliana na Injili ya utukufu wa Mungu anayehimidiwa, ambayo mimi nimewekewa amana.

*Neema Ya Mungu Kwa Paulo*

12 [l]Namshukuru Kristo Yesu Bwana wetu, aliyenitia nguvu, kwa sababu aliniona mwaminifu, akaniteua kwa kazi yake. 13 [m]Ingawa wakati fulani nilikuwa mwenye kukufuru, mtesaji na mwenye jeuri, lakini nilipata rehema kwa sababu nilitenda hivyo kwa kutojua na kutoamini kwangu. 14 [n]Neema ya Bwana wetu ilimiminwa juu yangu kwa wingi, ikiambatana na imani na upendo ulio katika Kristo Yesu.

15 [o]Msemo huu ni wa kweli na unaostahili kukubalika, usemao kwamba: Kristo Yesu alikuja ulimwenguni kuokoa wenye dhambi, ambao mimi ndiye niliye mbaya kuliko wote. 16 [p]Lakini kwa sababu hiyo nilipata rehema, ili katika mimi, niliyekuwa mwenye dhambi kuliko wote, Kristo Yesu apate kuonyesha uvumilivu wake usio na kikomo, ili niwe kielelezo kwa wale watakaomwamini na wapate uzima wa milele. 17 [q]Basi Mfalme wa milele, asiye na mwisho, asiyeonekana, aliye Mungu pekee, apewe heshima na utukufu milele na milele. Amen.

18 [r]Mwanangu Timotheo, ninakupa agizo hili, kwa kadiri ya maneno ya unabii yaliyosemwa kukuhusu, ili kwa kuyafuata upate kupigana vita vizuri, 19 [s]ukiishikilia imani na dhamiri njema, ambazo wengine wamevikataa, na hivyo wakaangamia kwa

---

[a]**1:1** Tit 1:3; Kol 1:27
[b]**1:2** Mdo 16:1; 1Kor 4:17; 1The 2:11
[c]**1:3** Mdo 18:19; Gal 1:6, 7
[d]**1:4** 1Tim 4:7; 2Tim 4:4; 1Tim 6:4
[e]**1:5** 2Tim 2:22; 1:5
[f]**1:6** 1Tim 6:4, 20
[g]**1:7** Efe 4:11; Ay 38:2
[h]**1:8** Rum 7:12
[i]**1:9** Gal 3:19; 5:23
[j]**1:10** 1Tim 6:3; 2Tim 1:13
[k]**1:11** 1The 2:4
[l]**1:12** Flp 4:13
[m]**1:13** Mdo 8:3; 26:9
[n]**1:14** Rum 5:20; 2Tim 1:13
[o]**1:15** 1Tim 4:9; 2Tim 2:11
[p]**1:16** 1Tim 1:13; Rum 2:4; Yn 3:15; Mt 25:46
[q]**1:17** Ufu 15:3; Kol 1:15; Rum 11:36
[r]**1:18** 1Tim 4:14; 2Tim 4:7
[s]**1:19** 1Tim 6:21; Mdo 23:1; 1Tim 6:21; 2Tim 2:18

habari ya imani yao. [20] [a]Miongoni mwao
wako Himenayo na Aleksanda, ambao
nimemkabidhi Shetani ili wafundishwe
wasije wakakufuru.

*Maagizo Kuhusu Kuabudu*

2 [b]Awali ya yote, nasihi kwamba dua, sala,
maombezi na shukrani zifanyike kwa
ajili ya watu wote: [2] [c]kwa ajili ya wafalme
na wale wote wenye mamlaka, ili tupate
kuishi kwa amani na utulivu, katika uchaji
wote wa Mungu na utakatifu. [3] [d]Jambo
hili ni jema, tena linapendeza machoni
pa Mungu Mwokozi wetu, [4] [e]anayetaka
watu wote waokolewe na wafikie kuijua
kweli. [5] [f]Kwa maana kuna Mungu mmoja
na mpatanishi mmoja kati ya Mungu na
wanadamu, yaani mwanadamu Kristo
Yesu, [6] [g]aliyejitoa mwenyewe kuwa fidia
kwa ajili ya wanadamu wote: jambo hili
lilishuhudiwa kwa wakati wake ufaao.
[7] [h]Nami kwa kusudi hili nimewekwa niwe
mhubiri na mtume (nasema kweli katika
Kristo wala sisemi uongo), mwalimu wa
watu wa Mataifa katika imani na kweli.

[8] [i]Nataka kila mahali wanaume wasali
wakiinua mikono mitakatifu pasipo hasira
wala kugombana.

[9] [j]Vivyo hivyo nataka wanawake
wajipambe kwa adabu na kwa heshima
katika mavazi yanayostahili, si kwa kusuka
nywele, kuvalia dhahabu, lulu au mavazi
ya gharama kubwa, [10] [k]bali kwa matendo
mazuri kama iwapasavyo wanawake
wanaokiri kuwa wanamcha Mungu.

[11] [l]Mwanamke na ajifunze kwa utulivu
na kwa utiifu wote. [12] [m]Simpi mwanamke
ruhusa ya kufundisha au kuwa na mamlaka
juu ya mwanaume. Mwanamke inampasa
kukaa kimya. [13] [n]Kwa maana Adamu
aliumbwa kwanza, kisha Eva. [14] [o]Wala si
Adamu aliyedanganywa, bali ni mwanamke
aliyedanganywa akawa mkosaji. [15] [p]Lakini
mwanamke ataokolewa kwa kuzaa kwake,
kama wakiendelea kudumu katika imani,
upendo na utakatifu, pamoja na kuwa na
kiasi.

*Sifa Za Waangalizi*

3 [q]Hili ni neno la kuaminiwa, kwamba mtu
akitamani kazi ya uangalizi, atamani
kazi nzuri. [2] [r]Basi, imempasa mwangalizi
awe mtu asiye na lawama, mume wa mke
mmoja, mwenye kiasi, anayejitawala,
anayeheshimika, mkarimu, ajuaye
kufundisha, [3] [s]asiwe mlevi, wala mkali bali
awe mpole, asiwe mgomvi wala mpenda
fedha. [4] [t]Lazima aweze kuisimamia nyumba
yake mwenyewe vizuri na kuhakikisha
kwamba watoto wake wanamtii na kuwa na
heshima kwa kila njia. [5] [u](Kwa maana kama
mtu hajui jinsi ya kusimamia nyumba yake
mwenyewe, atawezaje kuliangalia kanisa la
Mungu?) [6] [v]Asiwe mtu aliyeokoka karibuni
asije akajivuna na kuangukia kwenye
hukumu ile ile ya ibilisi. [7] [w]Inampasa pia
awe na sifa njema kwa watu walio nje, ili
asije akalaumiwa na kuanguka kwenye
mtego wa ibilisi.

*Sifa Za Mashemasi*

[8] [x]Vivyo hivyo, mashemasi nao wawe
watu wanaostahili heshima, wasiwe wenye
kauli mbili au wenye kujifurahisha kwa
mvinyo, wala wanaotamani faida isiyo
halali. [9] [y]Inawapasa kushikamana sana na

[a]**1:20** 2Tim 2:17; 4:14; 1Kor 5:5
[b]**2:1** Efe 6:18; Flp 4:6
[c]**2:2** Ezr 6:10; Rum 13:1
[d]**2:3** Mdo 20:1; 1Tim 5:4; Lk 1:42
[e]**2:4** Eze 18:23-32; 1Tim 4:10; 2Tim 2:25
[f]**2:5** Rum 10:12; Gal 3:20
[g]**2:6** 1Kor 1:6; 1Tim 6:15
[h]**2:7** 2Tim 1:11; Mdo 9:15; Efe 3:7-8
[i]**2:8** Za 24:4; Lk 24:50
[j]**2:9** 1Pet 3:3
[k]**2:10** 1Tim 5:10; Mit 31:13
[l]**2:11** 1Kor 14:34; 1Pet 3:3, 4
[m]**2:12** Efe 5:22; 1Kor 14:34; Mwa 3:16
[n]**2:13** Mwa 2:7, 22; 1Kor 11:8
[o]**2:14** Mwa 3:1-6, 13; 2Kor 11:3
[p]**2:15** 1Tim 1:14
[q]**3:1** 1Tim 1:15; Flp 1:1
[r]**3:2** Tit 1:6-8; Rum 12:13; 2Tim 2:24
[s]**3:3** 2Tim 2:24; Lk 16:14; 1Pet 5:2
[t]**3:4** Tit 1:6
[u]**3:5** 1Kor 10:32
[v]**3:6** 1Tim 6:4
[w]**3:7** 2Tim 2:26
[x]**3:8** Flp 1:1; Tit 2:3
[y]**3:9** 1Tim 1:9; Mdo 23:1

ile siri ya imani kwa dhamiri safi. 10 [a]Ni
lazima wapimwe kwanza; kisha kama
hakuna neno dhidi yao, basi na waruhusiwe
kuhudumu kama mashemasi.
11 [b]Vivyo hivyo, wake zao wawe wanawake
wanaostahili heshima, wasio wasingiziaji,
bali wawe na kiasi na waaminifu katika
kila jambo.
12 [c]Shemasi awe mume wa mke mmoja na
inampasa aweze kusimamia watoto wake
na watu wa nyumbani mwake vyema.
13 [d]Wale ambao wamehudumu vyema katika
huduma ya ushemasi hujipatia msimamo
bora na ujasiri mkubwa katika imani yao
ndani ya Kristo Yesu.
14 Ingawa ninatarajia kuja kwako hivi
karibuni, ninakuandikia maagizo haya sasa
ili kwamba, 15 [e]kama nikikawia, utajua jinsi
iwapasavyo watu kuenenda katika nyumba
ya Mungu, ambayo ndiyo kanisa la Mungu
aliye hai, lililo nguzo na msingi wa kweli.
16 [f]Bila shaka yoyote, siri ya utauwa ni
kubwa:

Alidhihirishwa katika mwili wa
kibinadamu,
akathibitishwa kuwa na haki
katika Roho,
akaonekana na malaika,
akahubiriwa miongoni mwa
mataifa,
akaaminiwa ulimwenguni,
akachukuliwa juu katika utukufu.

### *Maagizo Kwa Timotheo*

4 [g]Roho asema waziwazi kwamba katika
siku za mwisho baadhi ya watu wataiacha
imani na kufuata roho zidanganyazo na
mafundisho ya mashetani. 2 [h]Mafundisho
kama hayo huja kupitia kwa waongo ambao
ni wanafiki, hali dhamiri zao zikiungua
kwa kuchomwa moto. 3 [i]Wao huwakataza
watu wasioe na kuwaagiza wajiepushe
na vyakula fulani, ambavyo Mungu
aliviumba ili vipokewe kwa shukrani na
wale wanaoamini na kuijua kweli. 4 [j]Kwa
maana kila kitu alichokiumba Mungu ni
chema, wala hakuna kitu chochote cha
kukataliwa kama kikipokewa kwa shukrani,
5 [k]kwa sababu kimetakaswa kwa neno la
Mungu na kwa kuomba.

### *Mtumishi Mwema Wa Yesu Kristo*

6 [l]Kama ukiwakumbusha ndugu mambo
haya, utakuwa mtumishi mwema wa Kristo
Yesu, uliyelelewa katika kweli ya imani
na yale mafundisho mazuri uliyoyafuata.
7 [m]Usijishughulishe kamwe na hadithi
za kipagani na masimulizi ya uongo ya
wanawake wazee; badala yake, jizoeze
kuwa mtauwa. 8 [n]Kwa maana mazoezi
ya mwili yana faida kwa sehemu, lakini
utauwa una faida katika mambo yote,
yaani, unayo ahadi ya uzima wa sasa na
ya ule ujao.
9 [o]Hili ni neno la kuaminiwa tena lastahili
kukubaliwa kabisa, 10 [p](nasi kwa ajili ya
hili tunajitaabisha na kujitahidi), kwamba
tumeweka tumaini letu kwa Mungu aliye
hai, ambaye ni Mwokozi wa watu wote,
hasa wale waaminio.
11 [q]Mambo haya yaagize na kuyafundisha.
12 [r]Mtu yeyote asikudharau kwa kuwa
wewe ni kijana, bali uwe kielelezo kizuri
kwa waumini katika usemi, mwenendo,
upendo, imani na usafi. 13 [s]Fanya bidii
kusoma Maandiko hadharani, kuhubiri
na kufundisha, mpaka nitakapokuja.
14 [t]Usiache kutumia kipawa kilicho ndani

[a]**3:10** 1Tim 5:22
[b]**3:11** 2Tim 3:3; Tit 2:3
[c]**3:12** 1Tim 3:2, 4
[d]**3:13** Mt 25:21
[e]**3:15** 1Kor 10:32; Efe 2:21
[f]**3:16** Rum 16:25; Yn 1:14; Kol 1:23; Mk 16:19
[g]**4:1** Mdo 8:29; 2Tim 3:1; 1The 2:3
[h]**4:2** Efe 4:19
[i]**4:3** Ebr 13:4; Kol 2:16; Mwa 1:29; Rum 14:6
[j]**4:4** Rum 14:14-18
[k]**4:5** Ebr 4:12
[l]**4:6** 1Tim 1:10
[m]**4:7** 2Tim 2:16
[n]**4:8** 1Tim 6:6; Mit 22:4; Mt 6:33
[o]**4:9** 1Tim 1:15
[p]**4:10** 1Kor 4:11, 12; 1Tim 6:17; Za 36:6
[q]**4:11** 1Tim 5:7; 6:2
[r]**4:12** Flp 3:17; 1The 1:7; 1Tim 1:14
[s]**4:13** 1Tim 3:14; Lk 4:16; Mdo 13:14-16; Kol 4:16; 1The 5:27
[t]**4:14** 1Tim 1:18; Mdo 6:6; 2Tim 1:6

yako, ambacho ulipewa kwa neno la unabii
wakati wazee walikuwekea mikono.
15 Uwe na bidii katika mambo haya;
ujitolee kwa ajili ya mambo haya kikamilifu,
ili kila mtu aone kuendelea kwako.
16 [a]Jilinde sana nafsi yako na mafundisho
yako. Dumu katika hayo, kwa maana kwa
kufanya hivyo, utajiokoa wewe mwenyewe
pamoja na wale wanaokusikia.

### *Maagizo Kuhusu Wajane, Wazee Na Watumwa*

5 [b]Usimkemee mzee kwa ukali bali
umshawishi kama vile angekuwa ni baba
yako. Uwatendee vijana kama vile ndugu
zako; 2 nao wanawake wazee uwatendee
kama mama zako, na wanawake vijana
kama dada zako, katika usafi wote.
3 [c]Waheshimu wanawake wajane ambao
ni wajane kweli kweli. 4 [d]Kama mjane ana
watoto ama wajukuu, hawa inawapasa
awali ya yote wajifunze kutimiza wajibu
wao wa kumcha Mungu katika matendo
kwa kuwatunza wale wa jamaa zao
wenyewe, na hivyo wawarudishie wema
waliowatendea wazazi wao, kwa kuwa hivi
ndivyo impendezavyo Mungu. 5 [e]Mwanamke
ambaye ni mjane kweli kweli, yaani, yeye
aliyebaki peke yake huweka tumaini lake
kwa Mungu naye hudumu katika maombi
usiku na mchana akimwomba Mungu ili
amsaidie. 6 [f]Lakini mjane aishiye kwa anasa
amekufa, ingawa anaishi. 7 [g]Wape watu
maagizo haya pia, ili asiwepo yeyote wa
kulaumiwa. 8 [h]Kama mtu hawatunzi wale
wa jamaa yake, hasa wale wa nyumbani
mwake mwenyewe, ameikana imani, tena
ni mbaya kuliko yeye asiyeamini.
9 [i]Mjane yeyote asiwekwe kwenye orodha
ya wajane isipokuwa awe ametimiza umri
wa miaka sitini, na ambaye alikuwa mke wa
mume mmoja, 10 [j]awe ameshuhudiwa kwa
matendo yake mema, aliyewalea watoto
wake vizuri, aliye mkarimu, aliyewanawisha
watakatifu miguu, aliyewasaidia wenye
shida na aliyejitolea kwa ajili ya matendo
mema ya kila namna.
11 Lakini kwa habari za wajane vijana
usiwaweke kwenye orodha hiyo, maana
tamaa zao za kimaumbile zikizidi kule
kujitoa kwao kwa Kristo, watataka kuolewa
tena. 12 Nao kwa njia hiyo watajiletea
hukumu kwa kukiuka ahadi yao ya kwanza.
13 [k]Zaidi ya hayo, wajane kama hao huwa
na tabia ya uvivu wakizurura nyumba kwa
nyumba, wala hawawi wavivu tu, bali pia
huwa wasengenyaji, wajiingizao katika
mambo yasiyowahusu na kusema mambo
yasiyowapasa kusema. 14 [l]Hivyo nawashauri
wajane vijana waolewe, wazae watoto na
wasimamie nyumba zao, wasije wakampa
adui nafasi ya kutushutumu. 15 [m]Kwa maana
kwa kweli wajane wengine wamepotoka ili
kumfuata Shetani.
16 [n]Lakini kama mwanamke yeyote
aaminiye ana wajane katika jamaa yake,
inampasa awasaidie wala si kuwaacha
wakililemea kanisa, ili kanisa liweze
kuwasaidia wale ambao ni wajane kweli
kweli.

### *Wazee Wa Kanisa*

17 [o]Wazee wa kanisa wanaoongoza
shughuli za kanisa vizuri wanastahili
heshima mara mbili, hasa wale ambao
kazi yao ni kuhubiri na kufundisha. 18 [p]Kwa
maana Maandiko husema, “Usimfunge
maksai kinywa apurapo nafaka,” tena,
“Mfanyakazi anastahili mshahara wake.”
19 [q]Usiendekeze mashtaka dhidi ya mzee
isipokuwa yawe yameletwa na mashahidi

---

[a]**4:16** Rum 11:14; Mdo 20:28; Eze 33:9; 1Kor 9:22
[b]**5:1** Tit 2:2; Law 19:32; Tit 2:6
[c]**5:3** 1Tim 5:5, 16
[d]**5:4** Efe 6:1-2; Rum 12:2
[e]**5:5** 1Kor 7:34; 1Pet 3:5; Lk 2:37
[f]**5:6** Lk 15:24
[g]**5:7** 1Tim 4:11
[h]**5:8** Tit 1:16; Yud 4
[i]**5:9** Lk 2:36; 1Tim 3:2
[j]**5:10** Mdo 9:36; 1Pet 2:12; Lk 7:44
[k]**5:13** 2The 3:11
[l]**5:14** 1Kor 7:9; 1Tim 6:1
[m]**5:15** Mt 4:10
[n]**5:16** 1Tim 5:3, 5
[o]**5:17** Mdo 11:30; Flp 2:29; 1The 5:12
[p]**5:18** Kum 25:4; 1Kor 9:7-9; Law 19:13; Mt 10:10
[q]**5:19** Mdo 11:30; Mt 18:16

wawili au watatu. [20] [a]Wale wanaodumu katika dhambi uwakemee hadharani, ili wengine wapate kuogopa.

[21] [b]Ninakuagiza mbele za Mungu na mbele za Kristo Yesu na mbele za malaika wateule, shika maagizo haya pasipo ubaguzi wala upendeleo.

[22] [c]Usiwe na haraka kumwekea mtu mikono wala usishiriki dhambi za watu wengine. Jilinde nafsi yako uwe safi.

[23] [d]Acha kunywa maji peke yake, tumia divai kidogo kwa sababu ya tumbo lako na maumivu yako ya mara kwa mara.

[24] [e]Dhambi za watu wengine ni dhahiri nazo zinawatangulia kwenda hukumuni; na dhambi za watu wengine zinawafuata nyuma yao. [25] Vivyo hivyo, matendo mema yako dhahiri, na hata yale ambayo si mema hayawezi kufichika.

### *Watumwa*

6 [f]Wale wote walio chini ya kongwa la utumwa inawapasa kuwahesabu mabwana zao kuwa wanastahili heshima yote, ili jina la Mungu lisitukanwe wala mafundisho yetu. [2] [g]Wale watumwa ambao wana mabwana waaminio, haiwapasi kupunguza heshima yao kwa sababu wao ni ndugu. Badala yake, wawatumikie hata vizuri zaidi, kwa sababu wale wanaonufaika na huduma yao ni waaminio, ambao ni wapenzi wao. Fundisha mambo haya na uwahimize kuyafuata.

### *Mafundisho Ya Uongo Na Utajiri Wa Kweli*

[3] [h]Ikiwa mtu yeyote atafundisha mafundisho mapotovu wala hakubaliani na mafundisho manyofu ya Bwana wetu Yesu Kristo na yale ya utauwa, [4] [i]huyo amejivuna wala hajui kitu chochote. Yeye amejaa tamaa ya mabishano na ugomvi kuhusu maneno ambavyo matokeo yake ni wivu na mapigano, maneno ya ukorofi, shuku mbaya, [5] [j]na kuzozana kusikokoma kati ya watu walioharibika akili zao, walioikosa kweli, na ambao hudhani kwamba utauwa ni njia ya kupata faida.

[6] [k]Lakini utauwa na kuridhika ni faida kubwa. [7] [l]Kwa kuwa hatukuja humu duniani na kitu chochote, wala hatuwezi kutoka humu na kitu. [8] [m]Lakini kama tuna chakula na mavazi, tutaridhika navyo. [9] [n]Lakini wale watu wanaotamani kuwa na mali kwa haraka huanguka kwenye majaribu, na wamenaswa na tamaa nyingi za kipumbavu zenye kudhuru, zinazowazamisha watu katika uharibifu na maangamizi. [10] [o]Kwa maana kupenda fedha ndiyo shina moja la maovu ya kila namna. Baadhi ya watu wakitamani fedha, wameiacha imani na kujichoma wenyewe kwa maumivu mengi.

### *Vitu Vizuri Vya Imani*

[11] [p]Lakini wewe, mtu wa Mungu, yakimbie mambo haya yote. Fuata haki, utauwa, imani, upendo, saburi na upole. [12] [q]Pigana vile vita vizuri vya imani. Shika uzima wa milele ambao ndio ulioitiwa ulipokiri ule ukiri mzuri mbele ya mashahidi wengi. [13] [r]Nakuagiza mbele za Mungu avipaye vitu vyote uhai, na mbele za Kristo Yesu ambaye alipokuwa anashuhudia mbele ya Pontio Pilato alikiri ukiri mzuri, [14] [s]uishike amri hii bila dosari wala lawama mpaka kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo, [15] [t]ambaye Mungu atamleta kwa wakati wake mwenyewe: yeye ahimidiwaye, aliye peke yake Mtawala, Mfalme wa wafalme, na Bwana wa mabwana, [16] [u]yeye peke yake

---

[a]**5:20** 2Tim 4:2; Tit 1:13; Kum 13:11
[b]**5:21** 1Tim 6:13; 2Tim 4:1
[c]**5:22** Mdo 6:6; Efe 5:11
[d]**5:23** 1Tim 3:8
[e]**5:24** Gal 5:19
[f]**6:1** 1Pet 2:18; Tit 2:5-9
[g]**6:2** Efe 1:16; 1Tim 4:11
[h]**6:3** 1Tim 1:3-10
[i]**6:4** 2Tim 2:14
[j]**6:5** Tit 1:15
[k]**6:6** Flp 4:11; Ebr 13:5; 1Tim 4:8
[l]**6:7** Ay 1:21; Za 49:17
[m]**6:8** Mit 30:8; Ebr 13:5
[n]**6:9** Mit 15:27; 1Tim 3:7
[o]**6:10** Yak 5:19; 1Tim 3:3
[p]**6:11** 2Tim 3:10-17
[q]**6:12** 1Kor 9:25-26; 1Tim 1:18; Flp 3:12
[r]**6:13** 1Tim 1:11-17; Dan 2:47; Ufu 1:5
[s]**6:14** 1The 3:13; 1Kor 1:7; 2Tim 1:10; 4:1, 8
[t]**6:15** 1Tim 1:11-17; Dan 2:47; Ufu 1:5
[u]**6:16** Yn 1:18

ambaye hapatikani na mauti, na anakaa
katika nuru isiyoweza kukaribiwa, ambaye
hakuna mwanadamu aliyemwona wala
awezaye kumwona. Heshima na uweza una
yeye milele. Amen.
17 [a]Waagize wale ambao ni matajiri wa
ulimwengu huu waache kujivuna, wala
wasiweke tumaini lao katika mali ambayo si
ya hakika, bali waweke tumaini lao katika
Mungu ambaye hutupatia vitu vyote kwa
wingi ili tuvifurahie. 18 [b]Waagize watende
mema, wawe matajiri katika matendo
mema, pia wawe wakarimu na walio tayari
kushiriki mali zao na wengine. 19 [c]Kwa njia
hii watajiwekea hazina kama msingi kwa
ajili ya wakati ujao na hivyo watajipatia
uzima, yaani, ule uzima ambao ni wa kweli.

*Maelekezo Ya Binafsi Na Maombi Ya Baraka*

20 [d]Timotheo, linda kile kilichowekwa
amana kwako. Epuka majadiliano yasiyo
ya utauwa na mabishano ambayo kwa
uongo huitwa elimu, 21 [e]ambayo wengine
kwa kujidai kuwa nayo wameiacha imani.

Neema iwe nanyi. Amen.

---

[a]**6:17** Lk 12:20-21; 1Tim 4:10; Mdo 14:17
[b]**6:18** 1Tim 5:10; Rum 12:8-13
[c]**6:19** Mt 6:20
[d]**6:20** 2Tim 1:12-14; 2:16-18
[e]**6:21** Kol 4:18

# 2 TIMOTHEO

1 [a]Paulo mtume wa Kristo Yesu kwa
mapenzi ya Mungu, kulingana na ile
ahadi ya uzima uliomo ndani ya Kristo
Yesu.
2 [b]Kwa Timotheo, mwanangu mpendwa:
Neema, rehema na amani itokayo kwa
Mungu Baba, na kwa Kristo Yesu Bwana
wetu.

*Shukrani Na Kutiwa Moyo*

3 [c]Ninamshukuru Mungu, ninayemtumikia
kwa dhamiri safi, kama walivyofanya baba
zangu, ninapokukumbuka usiku na mchana
katika maombi yangu. 4 [d]Nikiyakumbuka
machozi yako, ninatamani sana kukuona
ili nipate kujawa na furaha. 5 [e]Nimekuwa
nikiikumbuka imani yako ya kweli,
waliokuwa nayo bibi yako Loisi na mama
yako Eunike na ambayo mimi ninasadiki
sasa wewe pia unayo. 6 [f]Kwa sababu hii
nakukumbusha uchochee ile karama
ya Mungu, iliyowekwa ndani yako
nilipokuwekea mikono yangu. 7 [g]Maana
Mungu hakutupa roho ya woga, bali roho
ya nguvu, ya upendo na ya moyo wa kiasi.
8 [h]Kwa hiyo usione haya kushuhudia
kuhusu Bwana wetu, wala usinionee haya
mimi niliye mfungwa kwa ajili yake. Bali
uishiriki pamoja nami taabu ya Injili, kwa
kadiri ya nguvu ya Mungu, 9 [i]ambaye
alituokoa na kutuita katika mwito mtakatifu:
si kwa kadiri ya matendo yetu mema bali
kwa sababu ya kusudi lake mwenyewe na
neema yake. Neema hii tulipewa katika
Kristo Yesu tangu milele. 10 [j]Lakini sasa
imefunuliwa kwa kudhihirishwa kwake
Mwokozi wetu, Kristo Yesu, ambaye
amebatilisha mauti na kuleta uzima na
kutokufa kwa njia ya Injili. 11 [k]Nami
nimewekwa kuwa mhubiri, mtume na
mwalimu wa Injili hii. 12 [l]Hii ndiyo sababu
ninateseka namna hii, lakini sioni haya kwa
maana ninamjua yeye niliyemwamini, na
kusadiki ya kuwa anaweza kukilinda kile
nilichokiweka amana kwake hadi siku ile.
13 [m]Shika kwa uthabiti kielelezo cha
mafundisho yenye uzima yale uliyoyasikia
kwangu, pamoja na imani na upendo
katika Kristo Yesu. 14 [n]Ilinde ile amana
uliyokabidhiwa kwa Roho Mtakatifu akaaye
ndani yetu.
15 [o]Unajua ya kuwa watu wote katika Asia
wameniacha, miongoni mwao wamo Filego
na Hermogene.
16 [p]Bwana akawahurumie watu wa
nyumbani mwa Onesiforo, kwa sababu
aliniburudisha mara kwa mara wala
hakuionea aibu minyororo yangu. 17 Badala
yake, alipokuwa Rumi, alinitafuta kwa bidii
mpaka akanipata. 18 [q]Bwana na amjalie
kupata rehema zake siku ile! Nawe unajua
vyema jinsi alivyonisaidia huko Efeso.

*Askari Mwema Wa Kristo Yesu*

2 [r]Basi, wewe mwanangu, uwe hodari
katika neema iliyo ndani ya Kristo
Yesu. 2 Nayo mambo yale uliyonisikia
nikiyasema mbele ya mashahidi wengi,
uwakabidhi watu waaminifu watakaoweza

[a]**1:1** 1Tim 6:19; Tit 1:2; 1Kor 1:1; Efe 3:6; Ebr 9:15
[b]**1:2** Mdo 16:1; 1Tim 1:2
[c]**1:3** Rum 1:10; Efe 1:16; Mdo 22:3; 23:1; 24:14; 27:23; Gal 1:14
[d]**1:4** Mdo 20:37; 2Tim 4:9; 4:21
[e]**1:5** 1Tim 1:5; 2Tim 3:15
[f]**1:6** Mdo 6:6; 1The 5:19; 1Tim 4:14
[g]**1:7** Yer 42:11; Rum 8:15; Lk 24:49; Mdo 1:8
[h]**1:8** Rum 1:16; Efe 3:1; 2Tim 2:3-9; 4:5
[i]**1:9** Rum 8:28; 1Tim 1:1; Tit 3:4; 1The 4:7; Ebr 3:1; Rum 3:20; 9:11; Tit 3:5
[j]**1:10** Efe 1:9; 1Kor 15:26, 54; Rum 16:26; Kol 1:26; Tit 1:3; 1Pet 1:20; Ebr 2:14
[k]**1:11** 1Tim 2:7; Mdo 9:15; Efe 3:7, 8; 2Tim 4:17
[l]**1:12** 1Tim 6:20; 1Kor 1:8; Efe 3:1; 2Tim 2:9; 1Pet 4:19; 1Tim 6:20; 2Tim 4:8
[m]**1:13** Tit 1:9; 1Tim 1:14
[n]**1:14** Rum 8:9; 1Tim 6:20; Rum 8:11
[o]**1:15** 2Tim 4:10-16, 19; Mdo 19:10
[p]**1:16** Mt 5:7; 2Tim 4:19; Flm 7; Mdo 28:20
[q]**1:18** Ebr 6:10; Mt 25:34-40; 2The 1:10; 1Tim 1:18
[r]**2:1** Efe 6:10; 1Tim 1:2; 2Tim 1:18

kuwafundisha watu wengine vilevile.
3 Vumilia taabu pamoja nasi kama askari
mwema wa Kristo Yesu. 4 Hakuna askari
yeyote ambaye akiwa vitani hujishughulisha
na mambo ya kawaida ya maisha haya
kwa sababu nia yake ni kumpendeza yule
aliyemwandika awe askari. 5 [a]Vivyo hivyo,
yeye ashindanaye katika michezo hawezi
kupewa tuzo ya ushindi asiposhindana
kulingana na kanuni za mashindano.
6 Mkulima mwenye bidii ya kazi ndiye
anayestahili kuwa wa kwanza kupata
fungu la mavuno. 7 Fikiri sana kuhusu
haya nisemayo, kwa maana Bwana atakupa
ufahamu katika mambo hayo yote.

8 [b]Mkumbuke Yesu Kristo, aliyefufuliwa
kutoka kwa wafu, yeye aliye wa uzao wa
Daudi. Hii ndiyo Injili yangu, 9 [c]ambayo
kwayo ninateseka hata kufikia hatua
ya kufungwa minyororo kama mhalifu.
Lakini neno la Mungu halifungwi. 10 [d]Kwa
hiyo ninavumilia mambo yote kwa ajili ya
wateule wa Mungu, kusudi wao nao wapate
wokovu ulio katika Kristo Yesu, pamoja na
utukufu wa milele.

11 [e]Hili ni neno la kuaminiwa:

Kwa maana kama tumekufa pamoja
naye,
tutaishi pia pamoja naye.
12 [f]Kama tukistahimili,
pia tutatawala pamoja naye.
Kama tukimkana yeye,
naye atatukana sisi.
13 [g]Kama tusipoamini,
yeye hudumu kuwa mwaminifu,
kwa maana hawezi kujikana
mwenyewe.

*Mfanyakazi Aliyekubaliwa Na Mungu*

14 [h]Endelea kuwakumbusha mambo
haya ukiwaonya mbele za Bwana waache
kushindana kwa maneno ambayo hayana
faida yoyote bali huwaangamiza tu wale
wanaoyasikia. 15 [i]Jitahidi kujionyesha
kwa Mungu kuwa umekubaliwa naye,
mtendakazi asiye na sababu ya kuona
aibu, ukilitumia kwa usahihi neno la
kweli. 16 [j]Jiepushe na maneno mabaya,
yasiyo na maana, yasiyo ya utauwa, kwa
maana hayo huzidi kuwatosa watu katika
kukosa heshima kwa Mungu. 17 [k]Mafundisho
yao yataenea kama kidonda kisichopona.
Miongoni mwao wamo Himenayo na Fileto
18 [l]ambao wameiacha kweli, wakisema
kwamba ufufuo wa wafu umekwisha
kuwako, nao huharibu imani ya baadhi
ya watu. 19 [m]Lakini msingi wa Mungu ulio
imara umesimama, ukiwa na muhuri wenye
maandishi haya: “Bwana anawajua walio
wake”; tena, “Kila alitajaye jina la Bwana,
na auache uovu.”

20 [n]Katika nyumba kubwa si kwamba
kuna vyombo vya dhahabu na fedha tu, bali
pia vimo vyombo vya miti na vya udongo;
vingine kwa matumizi maalum, na vingine
kwa matumizi ya kawaida. 21 [o]Basi ikiwa
mtu amejitakasa na kujitenga na hayo
niliyoyataja, atakuwa chombo maalum,
kilichotengwa na ambacho kinamfaa
mwenye nyumba, kimeandaliwa tayari kwa
kila kazi njema.

22 [p]Zikimbie tamaa mbaya za ujana,
ufuate haki, imani, upendo na amani
pamoja na wale wamwitao Bwana kwa
moyo safi. 23 [q]Jiepushe na mabishano ya
kipumbavu na yasiyo na maana, kwa kuwa
wajua ya kwamba hayo huzaa magomvi.
24 [r]Tena haimpasi mtumishi wa Bwana
kuwa mgomvi, bali inampasa awe mwema
kwa kila mtu, awezaye kufundisha, tena

[a]**2:5** 1Kor 9:25; 2Tim 4:8; 1Kor 9:10
[b]**2:8** Mdo 2:24; Rum 2:16
[c]**2:9** Mdo 9:16; 2Tim 1:12
[d]**2:10** Kol 1:24; 2Kor 4:17
[e]**2:11** Rum 6:2-11; 1Tim 1:15; 2Kor 4:10
[f]**2:12** Rum 8:17; 1Pet 4:13; Mt 10:33
[g]**2:13** Hes 23:19; 1Kor 1:9
[h]**2:14** 1Tim 5:21; 6:13; 2Tim 4:1; 1Tim 1:4; 6:4; Tit 3:9, 11
[i]**2:15** Kol 1:5; Yak 1:18
[j]**2:16** Tit 3:9; 1Tim 4:7; 6:20
[k]**2:17** 1Tim 1:20
[l]**2:18** 1Tim 6:21; 1Kor 15:12
[m]**2:19** Isa 28:16; Hes 16:5
[n]**2:20** 1Tim 3:15; Rum 9:21
[o]**2:21** 2Kor 9:8
[p]**2:22** 1Tim 6:11; 5:14
[q]**2:23** 1Tim 1:4; 4:7; 6:4; 2Tim 2:16; Tit 3:9; 2Tim 2:14
[r]**2:24** 1Tim 3:2-9; Tit 3:2; 1:9

mvumilivu. [25] [a]Inampasa kuwaonya kwa upole wale wanaopingana naye, kwa matumaini kwamba Mungu atawajalia kutubu na kuijua kweli, [26] [b]ili fahamu zao ziwarudie tena, nao waponyoke katika mtego wa ibilisi ambaye amewateka wapate kufanya mapenzi yake.

### *Hatari Za Siku Za Mwisho*

3 [c]Lakini yakupasa ufahamu jambo hili, kwamba siku za mwisho kutakuwa na nyakati za hatari. [2] [d]Kwa maana watu watakuwa wenye kujipenda wenyewe, wenye kupenda fedha, wenye kujisifu, wenye kiburi, wenye kumkufuru Mungu, wasiotii wazazi wao, wasio na shukrani, wasio watakatifu, [3] [e]wasio na upendo, wasiopenda kupatanishwa, wasingiziaji, wasiozuia tamaa zao, wakatili, wasiopenda mema, [4] [f]wasaliti, wakaidi, waliojaa majivuno, wapendao anasa zaidi kuliko kumpenda Mungu: [5] [g]wakiwa na mfano wa utauwa kwa nje, lakini wakizikana nguvu za Mungu. Jiepushe na watu wa namna hiyo.

[6] [h]Miongoni mwao wamo wale wajiingizao katika nyumba za watu na kuwachukua mateka wanawake wajinga, waliolemewa na dhambi zao na kuyumbishwa na aina zote za tamaa mbaya. [7] [i]Wakijifunza siku zote lakini kamwe wasiweze kufikia ujuzi wa kweli. [8] [j]Kama vile Yane na Yambre walivyopingana na Mose, vivyo hivyo watu hawa hupingana na ile kweli. Hawa ni watu wenye akili zilizopotoka, ambao wamekataliwa kwa mambo ya imani. [9] [k]Lakini hawataendelea sana, kwa sababu upumbavu wao utakuwa dhahiri kwa watu wote, kama ulivyokuwa dhahiri upumbavu wa hao watu wawili.

### *Paulo Amwagiza Timotheo*

[10] [l]Lakini wewe umeyajua mafundisho yangu, mwenendo, makusudi, imani, uvumilivu, upendo, ustahimilivu, [11] [m]mateso na taabu, yaani mambo yote yaliyonipata huko Antiokia, Ikonio na Listra, mateso yote niliyostahimili, lakini Bwana aliniokoa katika hayo yote. [12] [n]Naam, yeyote anayetaka kuishi maisha ya utauwa ndani ya Kristo Yesu atateswa. [13] [o]Lakini watu waovu na wadanganyaji watazidi kuwa waovu, wakidanganya na kudanganyika. [14] [p]Bali wewe, udumu katika yale uliyojifunza na kuyaamini kwa uthabiti, ukitambua ya kuwa ulijifunza hayo kutoka kwa nani, [15] [q]na jinsi ambavyo tangu utoto umeyajua Maandiko matakatifu, ambayo yanaweza kukuhekimisha upate wokovu kwa njia ya imani katika Kristo Yesu. [16] [r]Kila Andiko limevuviwa na Mungu na lafaa kwa mafundisho, kwa kuwaonya watu makosa yao, kwa kuwaongoza na kwa kuwafundisha katika haki, [17] [s]ili mtu wa Mungu awe amekamilishwa, apate kutenda kila kazi njema.

### *Maagizo Ya Mwisho*

4 [t]Nakuagiza mbele za Mungu na mbele za Kristo Yesu, atakayewahukumu watu walio hai na waliokufa wakati wa kuja kwake na ufalme wake, kwamba: [2] [u]Hubiri Neno; kuwa tayari wakati ufaao na wakati usiofaa; karipia, kemea na utie moyo kwa uvumilivu wote na kwa mafundisho

---

[a]**2:25** 1Tim 2:4; Gal 6:1; 1Tim 6:11; 1Pet 3:12; Mdo 8:22; 1Tim 2:4
[b]**2:26** 1Tim 3:7
[c]**3:1** 1Tim 4:1; 2Pet 3:3; 2Tim 4:3; 1Yn 2:18; Yud 18
[d]**3:2** 1Tim 3:3; Rum 1:30
[e]**3:3** Rum 1:31; 2Pet 3:3
[f]**3:4** 1Tim 3:6; 2Pet 2:10; Flp 3:19; 2Pet 2:13; Yud 4, 9
[g]**3:5** 1Tim 5:8; Tit 1:16; 2The 3:6; 1Tim 6:5
[h]**3:6** Yud 4; Mt 23:14; Tit 1:11
[i]**3:7** 1Tim 2:4; 2Tim 1:11
[j]**3:8** Kut 7:11; Mdo 13:8; 1Tim 6:5
[k]**3:9** Kut 8:18; 9:11; 7:12
[l]**3:10** 1Tim 4:6; Flp 2:22
[m]**3:11** Mdo 13:14, 50; 2Kor 11:23-27; Za 34:19
[n]**3:12** Mdo 14:22; Za 34:19; Mdo 14:22; Mt 16:24; Yos 17:14; 1Kor 15:19
[o]**3:13** 2Tim 2:16; 2The 2:11; 1Tim 4:1
[p]**3:14** 2Tim 1:13; 2:2
[q]**3:15** Yn 5:39; Za 119:98-99
[r]**3:16** 2Pet 1:20-21; Rum 4:23-24
[s]**3:17** 1Tim 6:11; 2Tim 2:21
[t]**4:1** Mdo 10:42; 1Tim 5:21
[u]**4:2** 1Tim 4:13; Gal 6:6; Tit 1:13; 2:15

mazuri. 3 [a]Maana wakati utakuja watu watakapokataa kuyakubali mafundisho yenye uzima. Badala yake, ili kutimiza tamaa zao wenyewe, watajikusanyia idadi kubwa ya walimu wapate kuwaambia yale ambayo masikio yao yanayowasha yanatamani kuyasikia.
4 [b]Watakataa kusikiliza kweli na kuzigeukia hadithi za uongo.
5 [c]Kwa habari yako wewe, vumilia mateso, fanya kazi ya mhubiri wa Injili, timiza wajibu wote wa huduma yako.

6 [d]Kwa maana mimi sasa ni tayari kumiminwa kama sadaka ya kinywaji, nayo saa yangu ya kuondoka imetimia.
7 [e]Nimevipiga vita vizuri, mashindano nimeyamaliza, imani nimeilinda.
8 [f]Sasa nimewekewa taji ya haki ambayo Bwana, mwamuzi wa haki, atanitunukia siku ile: wala si mimi tu, bali pia wote ambao wamengoja kwa shauku kudhihirishwa kwake.

*Maelekezo Ya Binafsi*

9 [g]Jitahidi kuja kwangu upesi
10 [h]kwa sababu Dema, kwa kuupenda ulimwengu, ameniacha na amekwenda Thesalonike. Kreske amekwenda Galatia na Tito amekwenda Dalmatia.
11 [i]Ni Luka peke yake aliye hapa pamoja nami. Mtafute Marko uje naye kwa sababu ananifaa sana katika huduma yangu.
12 [j]Nimemtuma Tikiko huko Efeso.
13 [k]Utakapokuja, niletee lile joho nililoliacha kwa Karpo huko Troa na vile vitabu vyangu, hasa vile vya ngozi.

14 [l]Aleksanda yule mfua chuma alinitendea ubaya mkubwa. Bwana atamlipa kwa ajili ya yale aliyotenda.
15 Wewe pia ujihadhari naye kwa sababu aliyapinga sana maneno yetu.

16 [m]Katika utetezi wangu wa mara ya kwanza, hakuna hata mmoja aliyeniunga mkono, bali kila mmoja aliniacha. Namwomba Mungu wasihesabiwe hatia kwa jambo hilo.
17 [n]Lakini Bwana alisimama upande wangu akanitia nguvu, ili kupitia kwangu lile Neno lihubiriwe kwa ukamilifu, watu wote Mataifa wapate kulisikia. Mimi niliokolewa kutoka kinywa cha simba.
18 [o]Bwana ataniokoa katika kila shambulio baya na kunileta salama katika Ufalme wake wa mbinguni. Atukuzwe yeye milele na milele. Amen.

*Salamu Za Mwisho*

19 [p]Wasalimu Prisila[q] na Akila, na wote wa nyumbani kwa Onesiforo.
20 [r]Erasto alibaki Korintho. Nami nikamwacha Trofimo huko Mileto akiwa mgonjwa.
21 [s]Jitahidi ufike huku kabla ya majira ya baridi. Eubulo anakusalimu, vivyo hivyo Pude, Lino, Klaudia na ndugu wote.

22 [t]Bwana awe pamoja na roho yako. Neema iwe pamoja nanyi. Amen.

---

[a]**4:3** 1Tim 1:4, 10; 2Tim 3:1, 6
[b]**4:4** 1Tim 1:4; 4:7; Tit 1:14
[c]**4:5** 2Tim 1:8; Mdo 21:8
[d]**4:6** Flp 2:17; 1:23; 2Pet 1:14
[e]**4:7** 1Tim 1:18; 1Kor 9:24
[f]**4:8** Kol 1:5; 2Tim 1:12
[g]**4:9** 2Tim 4:21; Tit 3:12
[h]**4:10** Kol 4:14; 1Yn 2:15; Mdo 16:6
[i]**4:11** Mdo 12:12; 2Tim 1:15; Kol 4:14; Flm 24; Mdo 12:25; Kol 4:10
[j]**4:12** Mdo 20:24; Efe 6:12; Kol 4:7; Tit 3:12
[k]**4:13** Mdo 16:8
[l]**4:14** Mdo 19:33; Za 28:4
[m]**4:16** Mdo 7:60; 2Tim 1:15
[n]**4:17** Mdo 23:11; 9:15
[o]**4:18** Za 121:7; Rum 11:36
[p]**4:19** Mdo 18:2; Rum 16; 3; 2Tim 1:16
[q]19 Prisila kwa Kiyunani ni Priska, hivyo tafsiri nyingine zimemuita Priska.
[r]**4:20** Mdo 19:22; 20:4
[s]**4:21** 2Tim 4:9; Tit 3:12
[t]**4:22** Gal 6:18; Flp 1:25; Kol 4:18

# TITO

1 [a]Paulo, mtumishi wa Mungu na mtume wa Yesu Kristo kwa ajili ya imani ya wateule wa Mungu na kuijua kweli iletayo utauwa: 2 [b]imani na ujuzi ulioko katika tumaini la uzima wa milele, ambao Mungu, asiyesema uongo, aliahidi hata kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, 3 [c]naye kwa wakati wake aliouweka alilidhihirisha neno lake kwa njia ya mahubiri ambayo mimi nimewekewa amana kwa amri ya Mungu Mwokozi wetu:

4 [d]Kwa Tito, mwanangu hasa katika imani tunayoshiriki sote:

Neema iwe kwako na amani itokayo kwa Mungu Baba na kwa Kristo Yesu Mwokozi wetu.

*Kazi Ya Tito Huko Krete*

5 [e]Sababu ya mimi kukuacha huko Krete ni ili uweke utaratibu mambo yale yaliyosalia na kuwaweka wazee wa kanisa katika kila mji, kama nilivyokuagiza. 6 [f]Mzee wa kanisa asiwe na lawama, awe mume wa mke mmoja, mtu ambaye watoto wake ni waaminio na wala hawashtakiwi kwa ufisadi. 7 [g]Kwa kuwa mwangalizi, kama wakili wa Mungu, imempasa kuwa mtu asiye na lawama, asiwe mwenye majivuno au mwepesi wa hasira, wala mlevi, wala asiwe mtu mwenye tamaa ya mapato yasiyo ya halali. 8 [h]Bali awe mkarimu, anayependa mema, mwenye kiasi, mwenye haki, mwadilifu, mnyofu, mtakatifu na mwenye kuitawala nafsi yake. 9 [i]Inampasa alishike kwa uthabiti lile neno la imani kama lilivyofundishwa, kusudi aweze kuwaonya wengine kwa mafundisho manyofu na kuwakanusha wale wanaopingana nayo.

*Walimu Wa Uongo*

10 [j]Kwa maana wako wengi wasiotii, wenye maneno yasiyo na maana, hasa wale wa kikundi cha tohara. 11 [k]Hao ni lazima wanyamazishwe, kwa sababu wanaharibu watu wa nyumba nzima wakifundisha mambo yasiyowapasa kufundisha. Wanafanya hivyo kwa ajili ya kujipatia mapato ya udanganyifu. 12 [l]Hata mmojawapo wa manabii wao mwenyewe amesema, "Wakrete ni waongo siku zote, wanyama wabaya, walafi, wavivu." 13 [m]Ushuhuda huu ni kweli. Kwa hiyo, uwakemee kwa ukali wapate kuwa wazima katika imani, 14 [n]ili wasiendelee kuangalia hadithi za Kiyahudi au maagizo ya wale watu wanaoikataa kweli. 15 [o]Kwa wale walio safi, kila kitu ni safi kwao. Lakini kwa wale waliopotoka na wasioamini, hakuna chochote kilicho safi. Kwa kweli nia zao na dhamiri zao zimepotoka. 16 [p]Wanadai kumjua Mungu, lakini kwa matendo yao wanamkana. Hao watu ni chukizo, wasiotii, wasiofaa kwa jambo lolote jema.

*Fundisha Mafundisho Manyofu*

2 [q]Inakupasa kufundisha itikadi sahihi. 2 [r]Wafundishe wazee kuwa na kiasi, wastahivu, wenye busara na wanyofu katika imani, upendo na saburi.

3 [s]Vivyo hivyo, wafundishe wanawake wazee kuwa na mwenendo wa utakatifu, wala wasiwe wasingiziaji au walevi,

---

[a]**1:1** Rum 1:1; 1Tim 2:4
[b]**1:2** 2Tim 1:1; 1:9
[c]**1:3** 1Tim 1:6; 2Tim 1:10; 1Tim 1:11; Lk 1:47
[d]**1:4** 2Kor 2:13; 1Tim 1:2; Rum 1:7; 1:12; 2Kor 4:13; Gal 2:3
[e]**1:5** Mdo 27:7; 11:30
[f]**1:6** 1Tim 3:2; 3:12; 4; 1The 3:13
[g]**1:7** 1Tim 3:1; 1Kor 4:1; 1Tim 3:3, 8
[h]**1:8** 1Tim 3:2; 2Tim 3:3
[i]**1:9** 1Kor 16:13; 1Tim 1:10
[j]**1:10** 1Tim 1:6; Mdo 11:2
[k]**1:11** 2Tim 3:6; Tit 3:6; Yn 10:12; 1Pet 5:2
[l]**1:12** Mdo 17:28; 2:11
[m]**1:13** 2Kor 13:10; Tit 2:2
[n]**1:14** 1Tim 4:7; 1:4; Kol 2:22; 2Tim 4:4
[o]**1:15** Rum 14:14, 23; Za 18:26; Mt 7:14-19; Mdo 10:9-16
[p]**1:16** 1Yn 2; 4; Yer 5; 2; 12:2; Hos 8:2, 3
[q]**2:1** 1Tim 1:10; 6:3; 2Tim 1:13
[r]**2:2** Tit 1:13; 1Tim 5:1; 3:2; Tit 2:5, 6, 12; 1:8, 13
[s]**2:3** 1Tim 3:8; 3:11

bali wafundishe yale yaliyo mema, 4 [a]ili
waweze kuwafundisha wanawake vijana
kuwa na kiasi, wawapende waume zao
na kuwapenda watoto wao, 5 [b]wawe
waaminifu, watakatifu, wakitunza vyema
nyumba zao, wema, watiifu kwa waume
zao, ili mtu yeyote asije akalikufuru neno
la Mungu.

6 [c]Vivyo hivyo, himiza vijana wawe na
kiasi. 7 [d]Katika kila jambo uwe kielelezo kwa
kutenda mema. Katika mafundisho yako
uonyeshe uadilifu, utaratibu, 8 [e]na usemi
sahihi usio na lawama, ili wanaokupinga
watahayari, wakose neno lolote baya la
kusema juu yetu.

9 [f]Wafundishe watumwa kuwatii
mabwana zao katika kila jambo, wakijitahidi
kuwapendeza wala wasijibizane nao,
10 [g]wala wasiwaibie, bali waonyeshe kuwa
wanaweza kuaminika kabisa, ili kwa kila
namna wayafanye mafundisho ya Mungu
Mwokozi wetu yawe ya kuvutia.

11 [h]Kwa maana neema ya Mungu ambayo
inawaokoa wanadamu wote imefunuliwa.
12 [i]Nayo yatufundisha kukataa ubaya na
tamaa za kidunia, ili tupate kuishi maisha ya
kiasi, ya haki na ya utaua katika ulimwengu
huu wa sasa, 13 [j]huku tukilitazamia tumaini
lenye baraka na ufunuo wa utukufu wa
Mungu wetu Mkuu, aliye Mwokozi wetu
Yesu Kristo. 14 [k]Ndiye alijitoa nafsi yake
kwa ajili yetu, ili atukomboe kutoka uovu
wote na kujisafishia watu kuwa mali yake
Mwenyewe, yaani, wale walio na juhudi
katika kutenda mema.

15 Basi wewe fundisha mambo haya.
Onya na kukaripia kwa mamlaka yote. Mtu
yeyote asikudharau.

*Kutenda Mema*

3 [l]Wakumbushe watu kuwanyenyekea
watawala na kuwatii wenye mamlaka,
wawe tayari kutenda kila lililo jema.
2 [m]Wasimnenee mtu yeyote mabaya, wasiwe
wagomvi, bali wawe wapole, wakionyesha
unyenyekevu kwa watu wote.

3 [n]Maana sisi wenyewe wakati fulani
tulikuwa wajinga, wasiotii, tukiwa watumwa
wa tamaa mbaya na anasa za kila aina.
Tuliishi katika uovu na wivu, tukichukiwa
na kuchukiana sisi kwa sisi. 4 [o]Lakini wema
na upendo wa Mungu Mwokozi wetu
ulipofunuliwa, 5 [p]alituokoa, si kwa sababu
ya matendo ya haki tuliyotenda, bali kwa
sababu ya rehema zake. Alituokoa kwa
kutuosha kwa kuzaliwa mara ya pili na
kwa kufanywa wapya kwa njia ya Roho
Mtakatifu, 6 [q]ambaye Mungu alitumiminia
kwa wingi kwa njia ya Yesu Kristo Mwokozi
wetu, 7 [r]ili kwamba, tukiisha kuhesabiwa
haki kwa neema yake, tupate kuwa warithi
tukiwa na tumaini la uzima wa milele.
8 [s]Hili ni neno la kuaminiwa. Nami nataka
uyasisitize mambo haya, ili wale ambao
wamemwamini Mungu wapate kuwa
waangalifu kujitoa kwa ajili ya kutenda
mema wakati wote. Mambo haya ni mazuri
tena ya manufaa kwa kila mtu.

9 [t]Lakini jiepushe na maswali ya kipuzi,
mambo ya koo, mabishano na ugomvi
kuhusu sheria, kwa sababu hayana faida,
tena ni ubatili. 10 [u]Mtu anayesababisha
mafarakano, mwonye mara ya kwanza,
kisha mwonye mara ya pili. Baada ya hapo,
usihusike naye tena. 11 [v]Kwa kuwa unajua
kwamba mtu kama huyo amepotoka na tena

[a]**2:4** 1Tim 5:2, 14
[b]**2:5** Efe 5:22; 1Tim 6:1
[c]**2:6** 1Tim 5:1
[d]**2:7** 1Tim 4:12; Tit 2:14
[e]**2:8** 1Pet 2:12; 1Tim 6:3; Neh 5:9; 1Tim 5:14; 2The 3:14
[f]**2:9** Efe 6:5; Kol 3:22; 1Tim 6:12; 1Pet 2:18; Efe 5:24
[g]**2:10** Mt 5:16; Flp 2:15; Tit 1:3; Lk 1:47
[h]**2:11** 1Tim 2:4; Rum 3:24; 2Tim 1:10
[i]**2:12** Tit 3:3; 2Tim 3:12
[j]**2:13** 2Pet 1:1; 1Kor 1:7; 1Tim 6:14; Flp 3:20
[k]**2:14** Za 85:4; Mit 16:7
[l]**3:1** Rum 13:1; 2Tim 2:21
[m]**3:2** Efe 4:31; 2Tim 2:24
[n]**3:3** Efe 2:2, 5, 8; 1Kor 6:11
[o]**3:4** Efe 2:7; Tit 2:11; Mit 8:31; 1Tim 2:3
[p]**3:5** Efe 2:9; Rum 12:2; 3:20; 9:11; Gal 2:16; 2Tim 1:9; Yn 3:3, 5
[q]**3:6** Rum 5:5; Eze 36:25; Yoe 2:28; Yn 1:16; Mdo 2:33; 10:45
[r]**3:7** Rum 3:24; 8:24; Tit 1:2
[s]**3:8** 1Tim 1:15; Tit 2:14
[t]**3:9** 1Tim 1:14; 2Tim 2:14
[u]**3:10** Rum 16:17; 2Kor 13:2; Mt 18:17; 2The 3:6, 14; 2Tim 3:5; Yn 10
[v]**3:11** Mdo 13:46; 1Tim 6:4, 5

ni mwenye dhambi. Yeye amejihukumu
mwenyewe.

*Maneno Ya Mwisho Na Kumtamkia Baraka*

12 [a]Mara nitakapomtuma Artema
au Tikiko kwako, jitahidi kuja unione
huko Nikopoli, kwa sababu nimeamua
kukaa huko wakati wa majira ya baridi.
13 [b]Fanya kila uwezalo uwasafirishe Zena
yule mwanasheria na Apolo na uhakikishe
kwamba wana kila kitu wanachohitaji
katika safari yao. 14 Watu wetu hawana
budi kujifunza kutenda mema, ili waweze
kuyakimu mahitaji ya kila siku, wasije
wakaishi maisha yasiyokuwa na matunda.
15 [c]Wote walio pamoja nami
wanakusalimu. Wasalimu wale
wanaotupenda katika imani.

Neema iwe nanyi nyote. Amen.

---

[a]**3:12** Mdo 20:4; 2Tim 4:9, 21
[b]**3:13** Mdo 18:24
[c]**3:15** 1Tim 1:2; Kol 4:18

# FILEMONI

1 [a]Paulo, mfungwa wa Kristo Yesu,
pamoja na Timotheo ndugu yetu:
Kwa Filemoni rafiki yetu mpendwa
na mtendakazi mwenzetu, 2 [b]kwa dada
yetu mpendwa Afia, kwa Arkipo askari
mwenzetu na kwa kanisa lile likutanalo
nyumbani mwako:
3 [c]Neema iwe nanyi na amani itokayo kwa
Mungu Baba yetu na Bwana Yesu Kristo.

*Shukrani Na Maombi*

4 [d]Siku zote ninamshukuru Mungu
ninapokukumbuka katika maombi yangu,
5 [e]kwa sababu ninasikia juu ya imani yako
katika Bwana Yesu na upendo wako kwa
watakatifu wote. 6 [f]Naomba utiwe nguvu
katika kuishuhudia imani yako, ili upate
kuwa na ufahamu mkamilifu juu ya kila
kitu chema tulicho nacho ndani ya Kristo.
7 [g]Upendo wako umenifurahisha mno na
kunitia moyo, kwa sababu wewe ndugu,
umeiburudisha mioyo ya watakatifu.

*Maombi Ya Paulo Ya Kumtetea Onesimo*

8 [h]Hata hivyo, ingawa katika Kristo
ningeweza kuwa na ujasiri na kukuagiza
yale yakupasayo kutenda, 9 [i]lakini
ninakuomba kwa upendo, mimi Paulo,
mzee na pia sasa nikiwa mfungwa wa
Kristo Yesu, 10 [j]nakuomba kwa ajili
ya mwanangu Onesimo,[k] aliyefanyika
mwanangu nilipokuwa kwenye minyororo.
11 Mwanzoni alikuwa hakufai, lakini sasa
anakufaa sana wewe na mimi pia.
12 Namtuma kwako, yeye aliye moyo
wangu hasa. 13 [l]Ningependa nikae naye ili
ashike nafasi yako ya kunisaidia wakati
huu nikiwa kifungoni kwa ajili ya Injili.
14 [m]Lakini sikutaka kufanya lolote bila idhini
yako, ili wema wowote uufanyao usiwe wa
lazima, bali wa hiari. 15 [n]Huenda sababu
ya yeye kutengwa nawe kwa kitambo
kidogo ni ili uwe naye daima. 16 [o]Si kama
mtumwa, bali bora kuliko mtumwa, kama
ndugu mpendwa. Yeye ni mpendwa sana
kwangu na hata kwako zaidi, yeye kama
mwanadamu na kama ndugu katika Bwana.
17 [p]Hivyo kama unanihesabu mimi kuwa
mshirika wako, mkaribishe kama vile
ungenikaribisha mimi mwenyewe. 18 [q]Kama
amekukosea lolote au kama unamdai
chochote, nidai mimi. 19 [r]Ni mimi Paulo,
ninayeandika waraka huu kwa mkono
wangu mwenyewe. Nitakulipa. Sitaji
kwamba nakudai hata nafsi yako. 20 [s]Ndugu
yangu, natamani nipate faida kwako katika
Bwana, uuburudishe moyo wangu katika
Kristo. 21 [t]Nikiwa na hakika ya utii wako,
nakuandikia, nikijua kwamba utafanya hata
zaidi ya yale ninayokuomba.
22 [u]Jambo moja zaidi: Niandalie chumba
cha wageni, kwa kuwa nataraji kurudishwa
kwenu kama jibu la maombi yenu.

*Salamu Za Mwisho Na Dua Ya Kuwatakia Heri*

23 [v]Epafra, aliye mfungwa mwenzangu
katika Kristo Yesu, anakusalimu. 24 [w]Vivyo
hivyo Marko, Aristarko, Dema na Luka,
watendakazi wenzangu wanakusalimu.

---

[a]**1:1** Efe 3:1; 2Kor 1:1; Flp 2:25
[b]**1:2** Kol 4:17; Flp 2:25; Rum 16:5
[c]**1:3** Rum 1:7; Efe 1:2
[d]**1:4** Rum 1:8; 1:10; Efe 1:16; 1The 1:2; 2The 1:2
[e]**1:5** 2Tim 2:22; Mdo 23:1; 1Tim 4:2; Gal 5:23
[f]**1:6** Flp 1:9, 11
[g]**1:7** 2Kor 7:4, 13; 7:4, 13; 2Tim 1:16; Flm 20
[h]**1:8** 1The 2:6
[i]**1:9** Efe 3:1; Flm 1, 23; 1Kor 1:10
[j]**1:10** 1Kor 4:15; 1The 2:11
[k]10 *Onesimo* maana yake ni *Wa manufaa.*
[l]**1:13** Flm 10; Mdo 21:33; 1Kor 16:17; Flp 2:20; Kol 4:9
[m]**1:14** 2Kor 9:7; 1Pet 5:2
[n]**1:15** Mwa 45:5, 8
[o]**1:16** Mt 23:8; Mdo 1:16
[p]**1:17** 2Kor 8:23
[q]**1:18** Mwa 43:9
[r]**1:19** 1Kor 16:21; Gal 6:11; 2The 3:17
[s]**1:20** 1Kor 16:18; Flm 7
[t]**1:21** 2Kor 2:3; 1Kor 7:16
[u]**1:22** Flp 2:24; Ebr 13:19; Flp 1:19
[v]**1:23** Kol 1:17
[w]**1:24** Mdo 12:12; 19:29; 2Tim 4:10

25 [a]Neema ya Bwana Yesu Kristo iwe
pamoja na roho zenu. Amen.

[a]**1:25** 2Tim 4:22

# WAEBRANIA

*Mwana Ni Mkuu Kuliko Malaika*

1 [a]Zamani Mungu alisema na baba zetu
kwa njia ya manabii mara nyingi na
kwa njia mbalimbali, 2 [b]lakini katika siku
hizi za mwisho anasema nasi kwa njia ya
Mwanawe, ambaye amemweka kuwa mrithi
wa vitu vyote, na ambaye kupitia kwake
aliuumba ulimwengu. 3 [c]Mwana ni mng'ao
wa utukufu wa Mungu na mfano halisi wa
nafsi yake, akivihifadhi vitu vyote kwa
neno lake lenye uweza. Akiisha kufanya
utakaso kwa ajili ya dhambi, aliketi mkono
wa kuume wa Aliye Mkuu huko mbinguni.
4 [d]Kwa hiyo alifanyika bora kuliko malaika,
kama jina alilorithi lilivyo bora kuliko lao.
5 [e]Kwa maana ni malaika yupi ambaye
wakati wowote Mungu alipata kumwambia,

"Wewe ni Mwanangu;
leo mimi nimekuzaa?"

Au tena,

"Mimi nitakuwa Baba yake,
naye atakuwa Mwanangu?"

6 [f]Tena, Mungu amletapo mzaliwa wake wa
kwanza ulimwenguni, anasema,

"Malaika wote wa Mungu na
wamsujudu."

7 [g]Anenapo kuhusu malaika asema,

"Huwafanya malaika wake kuwa
pepo,
watumishi wake kuwa miali ya
moto."

8 [h]Lakini kwa habari za Mwana asema,

"Kiti chako cha enzi, Ee Mungu,
kitadumu milele na milele,
nayo haki itakuwa fimbo ya utawala
ya ufalme wako.
9 [i]Umependa haki na kuchukia uovu;
kwa hiyo Mungu, Mungu wako,
amekuweka juu ya wenzako
kwa kukupaka mafuta ya furaha."

10 [j]Pia asema,

"Hapo mwanzo, Ee Bwana, uliweka
misingi ya dunia,
nazo mbingu ni kazi ya mikono
yako.
11 [k]Hizo zitatoweka, lakini wewe
utadumu;
zote zitachakaa kama vazi.
12 [l]Utazikung'utakung'uta kama joho,
nazo zitachakaa kama vazi.
Lakini wewe hubadiliki,
nayo miaka yako haikomi
kamwe."

13 [m]Je, ni kwa malaika yupi ambaye Mungu
amepata kumwambia wakati wowote,

"Keti mkono wangu wa kuume,
hadi nitakapowaweka adui zako
chini ya miguu yako"?

14 [n]Je, malaika wote si roho watumikao,
waliotumwa kuwahudumia wale
watakaourithi wokovu?

---

[a]**1:1** Efe 3:1; 2Kor 1:1; Hes 12:6, 8; Yn 9:29; Ebr 2:3; 4:8; 12:25; Lk 1:70; Mdo 2:30
[b]**1:2** Kum 4:30; Ebr 9:26; 1Pet 1:20; Ebr 1:5; Mt 3:17; Ebr 3:6; 5:8; 7:28; Za 2:8; Mt 28:18; Yn 1:3; Ebr 11:3
[c]**1:3** Yn 1:14; 14:9; Kol 1:17; Tit 2:14; Ebr 7:27; Mk 16:19
[d]**1:4** Efe 1:21; Flp 2:9, 10; Ebr 8:6
[e]**1:5** Za 2:7; Mt 3:17; 2Sam 7:14
[f]**1:6** Yn 3:16; Kol 1:18; Ebr 10:5; Kum 32:43; Za 97:7
[g]**1:7** Za 104:4
[h]**1:8** Lk 1:33; Za 45:6, 7
[i]**1:9** Flp 2:9; Isa 61:1, 3; Za 45:6, 7; Mdo 4:27; 10:38
[j]**1:10** Za 8:6; 102:25; Zek 12:1
[k]**1:11** Isa 34:4; 51:6; Ebr 12:27; Mt 24:35; 2Pet 3:7; 3:10; Ufu 21:1
[l]**1:12** Ebr 13:8; Za 102:25, 27
[m]**1:13** Ebr 1:3; Mk 16:19; Yos 10:24; Ebr 10:13; Za 110:1; Mt 22:44
[n]**1:14** Za 91:11; 103:20; Dan 7:10; Mt 25:34; Mk 10:17; Mdo 20:32; Rum 11:14; Ebr 2:3; 5:9; 9:28

*Wokovu Mkuu*

2 [a]Kwa hiyo, imetupasa kuwa waangalifu
sana kuhusu kile tulichosikia, ili tusije
tukakiacha. 2 [b]Kwa kuwa kama ujumbe
ulionenwa na malaika ulikuwa imara, na
kila uasi na kutokutii kulipata adhabu
ya haki, 3 [c]je, sisi tutapaje kupona kama
tusipojali wokovu mkuu namna hii?
Wokovu huu, ambao mwanzo ulitangazwa
na Bwana, ulithibitishwa kwetu na wale
waliomsikia. 4 [d]Pia Mungu aliushuhudia
kwa ishara, maajabu na kwa miujiza
mbalimbali, na karama za Roho Mtakatifu
alizozigawa kulingana na mapenzi yake.

*Yesu Alifananishwa Na Ndugu Zake*

5 [e]Mungu hakuuweka ulimwengu ujao
ambao tunanena habari zake chini ya
malaika. 6 [f]Lakini kuna mahali mtu fulani
ameshuhudia akisema:

“Mwanadamu ni kitu gani hata
unamfikiria,
binadamu ni nani hata unamjali?
7 Umemfanya chini kidogo kuliko
malaika;
ukamvika taji ya utukufu na
heshima,
8 [g]nawe umeweka vitu vyote chini
ya miguu yake.”

Kwa kuweka vitu vyote chini yake,
Mungu hakuacha kitu chochote ambacho
hakukiweka chini ya mwanadamu. Lakini
kwa sasa, hatuoni kwamba kila kitu kiko
chini yake. 9 [h]Lakini twamwona Yesu,
aliyefanywa chini kidogo kuliko malaika,
sasa akiwa amevikwa taji ya utukufu na
heshima kwa sababu alistahimili mauti,
ili kwamba kwa neema ya Mungu apate
kuonja mauti kwa ajili ya kila mtu.
10 [i]Ili kuwaleta wana wengi katika
utukufu, ilifaa kwamba Mungu, ambaye
ni kwa ajili yake na kupitia kwake kila kitu
kimekuwepo, amkamilishe mwanzilishi wa
wokovu wao kwa njia ya mateso. 11 [j]Yeye
awafanyaye watu kuwa watakatifu, pamoja
na hao ambao hufanywa watakatifu, wote
hutoka katika jamaa moja. Hivyo Yesu
haoni aibu kuwaita ndugu zake. 12 [k]Yeye
husema,

“Nitalitangaza jina lako kwa ndugu
zangu;
mbele ya kusanyiko nitaimba sifa
zako.”

13 [l]Tena,

“Nitaweka tumaini langu kwake.”

Tena anasema,

“Niko hapa, pamoja na watoto
ambao Mungu amenipa.”

14 [m]Basi kwa kuwa watoto wana nyama
na damu, yeye pia alishiriki katika
ubinadamu wao, ili kwa kifo chake, apate
kumwangamiza huyo mwenye nguvu za
mauti, yaani ibilisi, 15 [n]na kuwaweka huru
wale waliokuwa utumwani maisha yao
yote kwa sababu ya kuogopa mauti. 16 [o]Kwa
kuwa ni dhahiri kwamba hakuja kusaidia
malaika, bali uzao wa Abrahamu. 17 [p]Kwa
sababu hii ilibidi afanane na ndugu zake
kwa kila hali, ili apate kuwa Kuhani Mkuu
mwenye huruma na mwaminifu katika
kumtumikia Mungu, ili pia apate kufanya
upatanisho kwa ajili ya dhambi za watu.

---

[a]**2:1** Rum 11:22
[b]**2:2** Ebr 1:1; Kum 33:2; Mdo 7:53; Gal 3:19; Ebr 10:28
[c]**2:3** Ebr 10:29; 12:25; 1:2; Lk 1:2
[d]**2:4** Mk 16:20; Yn 4:48; 1Kor 12:4; Efe 1:5
[e]**2:5** Ebr 6:5; 2Pet 3:13
[f]**2:6** Ebr 4:4; Ay 7:17; Za 144:3; 8:4-6
[g]**2:8** Za 8:4-6; Mt 22:44; 28:18; 1Kor 15:27; Efe 1:22; Ebr 1:13; 1Kor 15:2
[h]**2:9** Ebr 2:7; Mdo 3:13; Flp 2:7-9; 2Kor 5:15; Mdo 2:33; Yn 3:16; 12:32; Rum 5:18; 8:32; 2Kor 5:15; 1Tim 2:6; 1Yn 2:2; Ufu 5:9
[i]**2:10** Rum 11:36; Lk 24:26; Ebr 5:8, 9; 7:28; Lk 24:46; Mdo 3:15; 5:31; Ebr 12:2; Lk 13:32; Ebr 5:9
[j]**2:11** Ebr 10:10; Mdo 17:26; Mt 28:10; Yn 20:17; Rum 8:29; Efe 5:26; Ebr 13:12
[k]**2:12** Za 22:22, 25; 68:26
[l]**2:13** Isa 8:17, 18; Yn 10:29; Za 18:2; Isa 12:2; Yn 20:17; 17:6, 9, 11, 12
[m]**2:14** Yn 1:14; Rum 8:3
[n]**2:15** 2Tim 1:7; Lk 1:74; Rum 8:15
[o]**2:16** Isa 41:8, 9; Lk 3:8
[p]**2:17** Ebr 2:14; 5:1; 5:2; 3:1; 4:14, 15; Flp 2:7; Rum 3:25; Za 22:22

18 [a]Kwa kuwa yeye mwenyewe aliteswa
alipojaribiwa, aweza kuwasaidia wale
wanaojaribiwa.

*Yesu Ni Mkuu Kuliko Mose*

3 [b]Kwa hiyo ndugu watakatifu, mnaoshiriki
mwito wa mbinguni, mtafakarini
Yesu, mtume na Kuhani Mkuu wa ukiri
wetu. 2 [c]Alikuwa mwaminifu kwa yeye
aliyemweka, kama vile Mose alivyokuwa
mwaminifu katika nyumba yote ya Mungu.
3 [d]Yesu ameonekana anastahili heshima
kubwa kuliko Mose, kama vile mjenzi wa
nyumba alivyo wa heshima kubwa kuliko
nyumba yenyewe. 4 [e]Kwa kuwa kila nyumba
hujengwa na mtu fulani, lakini Mungu ni
mjenzi wa kila kitu. 5 [f]Basi Mose kama
mtumishi alikuwa mwaminifu katika
nyumba yote ya Mungu, akishuhudia
kwa yale ambayo yangetamkwa baadaye.
6 [g]Lakini Kristo ni mwaminifu kama Mwana
katika nyumba ya Mungu. Sisi ndio nyumba
yake, kama tutashikilia sana ujasiri wetu
na tumaini tunalojivunia.

*Onyo Dhidi Ya Kutokuamini*

7 [h]Kwa hiyo, kama Roho Mtakatifu
asemavyo:

“Leo, kama mkiisikia sauti yake,
8 [i]msiifanye mioyo yenu migumu,
kama mlivyofanya katika uasi,
wakati ule wa kujaribiwa
jangwani,
9 [j]ambapo baba zenu walinijaribu na
kunipima
ingawa kwa miaka arobaini
walikuwa wameyaona matendo
yangu.
10 Hiyo ndiyo sababu nilikasirikia
kizazi kile,
nami nikasema, ‘Siku zote mioyo
yao imepotoka,
nao hawajazijua njia zangu.’
11 [k]Hivyo nikatangaza kwa kiapo katika
hasira yangu,
‘Kamwe hawataingia rahani
mwangu.’ ”

12 [l]Ndugu zangu, angalieni, asiwepo
miongoni mwenu mtu mwenye moyo
mwovu usioamini, unaojitenga na Mungu
aliye hai. 13 [m]Lakini mtiane moyo mtu na
mwenzake kila siku, maadamu iitwapo
Leo, ili asiwepo hata mmoja wenu mwenye
kufanywa mgumu kwa udanganyifu wa
dhambi. 14 [n]Kwa kuwa tumekuwa washiriki
wa Kristo, kama tukishikamana tu kwa
uthabiti na tumaini letu la kwanza hadi
mwisho. 15 [o]Kama ilivyonenwa:

“Leo, kama mkiisikia sauti yake,
msiifanye mioyo yenu migumu
kama mlivyofanya wakati wa kuasi.”

16 Basi ni nani waliosikia lakini bado
wakaasi? Je, si wale wote waliotoka
Misri wakiongozwa na Mose? 17 Lakini
ni nani aliowakasirikia miaka arobaini?
Je, si wale waliofanya dhambi ambao
miili yao ilianguka jangwani? 18 Ni nani
hao ambao Mungu aliapa kuwa kamwe
hawataingia rahani mwake isipokuwa ni
wale waliokataa kutii? 19 Hivyo tunaona
kwamba hawakuweza kuingia kwa sababu
ya kutokuamini kwao.

[a]**2:18** Ebr 4:15, 16; 5:2; 7:2; 4:15
[b]**3:1** Ebr 2:11; Rum 8:28; 2:17; 1Tim 6:12; Ebr 4:14; 10:23
[c]**3:2** Hes 12:7; Ebr 3:5
[d]**3:3** Kum 34:12; Zek 6:12; Mt 16:18
[e]**3:4** Efe 2:10; 3:9; Ebr 1:2; Mwa 1:1
[f]**3:5** Kut 14:31; Ebr 3:2; Hes 12:7; Kum 3:24; 8:15; 18:9; Yos 1:2; 8:31
[g]**3:6** Ebr 1:2; 6:11, 18, 19; 7:19; 11:1; 1Kor 3:16; 1Tim 3:15; Rum 11:22; 5:2; Hes 4:14
[h]**3:7** Mdo 28:25; Ebr 9:8; 10:15
[i]**3:8** Ebr 3:15; 4:7
[j]**3:9** Hes 14:33; Kum 1:3; Mdo 7:36
[k]**3:11** Kum 1:34, 35; Ebr 4:3, 5; Za 95:7-11
[l]**3:12** Mt 16:16
[m]**3:13** Ebr 10:24, 25; Yer 17:9; Efe 4:22
[n]**3:14** Efe 3:12; Ebr 3:6
[o]**3:15** Za 95:7, 8; Ebr 4:7; 3:7, 8

*Pumziko Aliloahidi Mungu*

4 [a]Kwa hiyo, kwa kuwa bado ahadi ya
kuingia rahani iko wazi, tujihadhari ili
hata mmoja wenu asije akaikosa. 2 [b]Kwa
maana sisi pia tumesikia Injili iliyohubiriwa
kwetu, kama nao walivyosikia; lakini
ujumbe ule waliousikia haukuwa na
maana kwao, kwa sababu wale waliousikia
hawakuuchanganya na imani. 3 [c]Sasa sisi
ambao tumeamini tunaingia katika ile raha,
kama vile Mungu alivyosema,

> “Kwa hiyo nikaapa katika hasira
> yangu,
> ‘Kamwe hawataingia rahani
> mwangu.’ ”

Lakini kazi yake ilikamilika tangu kuumbwa
kwa ulimwengu. 4 [d]Kwa maana mahali
fulani amezungumza kuhusu siku ya saba,
akisema: “Katika siku ya saba Mungu
alipumzika kutoka kazi zake zote.” 5 [e]Tena
hapo juu asema, “Kamwe hawataingia
rahani mwangu.”
6 [f]Kwa hiyo inabaki kuwa wazi kwa
wengine kuingia, nao wale wa kwanza
waliopokea Injili walishindwa kuingia kwa
sababu ya kutokutii. 7 [g]Kwa hiyo Mungu
ameweka siku nyingine, akaiita Leo,
akisema kwa kinywa cha Daudi baadaye
sana, kwa maneno yaliyotangulia kunenwa:

> “Leo, kama mkiisikia sauti yake,
> msiifanye mioyo yenu migumu.”

8 [h]Kwa maana kama Yoshua alikuwa
amewapa raha, Mungu hangesema tena
baadaye kuhusu siku nyingine. 9 Kwa
hiyo basi, imebaki raha ya Sabato kwa
ajili ya watu wa Mungu; 10 [i]kwa kuwa kila
mmoja aingiaye katika raha ya Mungu pia
hupumzika kutoka kazi zake mwenyewe,
kama vile Mungu alivyopumzika kutoka
kazi zake. 11 [j]Basi, na tufanye bidii kuingia
katika raha hiyo, ili kwamba asiwepo
yeyote atakayeanguka kwa kufuata mfano
wao wa kutokutii.
12 [k]Kwa maana Neno la Mungu li hai
tena lina nguvu. Lina makali kuliko
upanga wowote wenye makali kuwili,
hivyo linachoma hata kuzigawanya nafsi
na roho, viungo na mafuta yaliyo ndani
yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo
na makusudi ya moyo. 13 [l]Wala hakuna
kiumbe chochote kilichofichika machoni
pa Mungu. Kila kitu kimefunuliwa na kiko
wazi machoni pake yeye ambaye kwake ni
lazima tutatoa hesabu.

*Yesu Kristo Kuhani Mkuu Kuliko Wote*

14 [m]Kwa kuwa tunaye Kuhani Mkuu kuliko
wote ambaye ameingia mbinguni, Yesu
Mwana wa Mungu, basi na tushikamane
sana kwa uthabiti na ule ukiri wa imani
yetu. 15 [n]Kwa kuwa hatuna Kuhani Mkuu
asiyeweza kuchukuliana na sisi katika
udhaifu wetu, lakini tunaye mmoja ambaye
alijaribiwa kwa kila namna, kama vile
sisi tujaribiwavyo: lakini yeye hakutenda
dhambi. 16 [o]Basi na tukikaribie kiti cha
rehema kwa ujasiri, ili tupewe rehema na
kupata neema ya kutusaidia wakati wa
mahitaji.

5 [p]Kwa maana kila kuhani mkuu
anayechaguliwa miongoni mwa
wanadamu anawekwa kuwawakilisha
kwa mambo yanayomhusu Mungu, ili
apate kutoa matoleo na dhabihu kwa ajili
ya dhambi. 2 [q]Kwa kuwa yeye mwenyewe
ni dhaifu, aweza kuwachukulia kwa upole

[a]**4:1** Ebr 12:15
[b]**4:2** 1The 2:13
[c]**4:3** Za 95:11; Kum 1:34, 35; Ebr 3:11
[d]**4:4** Mwa 2:2, 3; Kut 20:11
[e]**4:5** Za 95:11; Ebr 3:3
[f]**4:6** Ebr 5:1; 3:18
[g]**4:7** Za 95:7, 8; Ebr 3:7
[h]**4:8** Yos 22:4; Ebr 1:1
[i]**4:10** Law 23:3; Ufu 14:13; Ebr 5:4
[j]**4:11** Ebr 5:6; 3:18
[k]**4:12** Mk 4:14; 5:1; 11:28; Yn 10:35; Mdo 12:24; 1The 2:13; Isa 55:11; Yer 23:29; Ufu 1:16; 1Kor 14:24, 25
[l]**4:13** Za 33:13-15; Mit 5:21; Yer 16:17; 23:24; Dan 2:22
[m]**4:14** Ebr 2:17; 6:20; 8:1; 9:2; Mt 4:3; Ebr 3:1
[n]**4:15** Ebr 2:17, 18; 2Kor 5:21; Isa 53:3; Lk 22:28; 1Pet 2:22; 1Yn 3:5; Ebr 7:26
[o]**4:16** Ebr 7:19; Efe 2:18; 3:12; Ebr 10:19
[p]**5:1** Ebr 2:17; 8:3; 9:9-27
[q]**5:2** Ebr 2:18; 4:15; 7:28

wale wasiojua na kupotoka. 3 [a]Hii ndiyo
sababu inampasa kutoa dhabihu kwa ajili
ya dhambi zake mwenyewe na vivyo hivyo
kwa ajili ya dhambi za watu. 4 [b]Hakuna
anayejitwalia heshima hii mwenyewe; ni
lazima aitwe na Mungu, kama vile Aroni
alivyoitwa. 5 [c]Pia Kristo hakujitwalia
utukufu yeye mwenyewe wa kuwa Kuhani
Mkuu, bali Mungu alimwambia,

> "Wewe ni Mwanangu;
> leo mimi nimekuzaa."

6 [d]Pia mahali pengine asema,

> "Wewe ni kuhani milele,
> kwa mfano wa Melkizedeki."

7 [e]Katika siku za maisha ya Yesu hapa
duniani, alimtolea maombi na dua pamoja
na kulia sana na machozi, yeye awezaye
kumwokoa na mauti, naye Mungu
akamsikia kwa sababu ya kutii kwake kwa
unyenyekevu. 8 [f]Ingawa alikuwa Mwana,
alijifunza utiifu kutokana na mateso
aliyoyapata, 9 [g]na akiisha kukamilishwa,
akawa chanzo cha wokovu wa milele kwa
wote wanaomtii. 10 [h]Naye amewekwa na
Mungu kuwa Kuhani Mkuu kwa mfano wa
Melkizedeki.

*Wito Wa Kukua Kiroho*

11 [i]Tunayo mengi ya kusema kuhusu
habari ya ukuhani huu, lakini ni vigumu
kuyaeleza, kwa sababu ninyi ni wazito wa
kuelewa. 12 [j]Kwa hakika, ingawa mpaka
wakati huu ingewapasa kuwa walimu,
bado mnahitaji mtu wa kuwafundisha tena
hatua za awali za kweli ya Neno la Mungu.
Mnahitaji maziwa, wala si chakula kigumu!
13 [k]Kwa maana yeyote aishiye kwa kunywa
maziwa bado yeye ni mtoto mchanga, hana
ujuzi katika mafundisho kuhusu neno la
haki. 14 [l]Lakini chakula kigumu ni kwa ajili
ya watu wazima, ambao kwa kujizoeza
wamejifunza kupambanua kati ya mema
na mabaya.

*Hatari Ya Kuanguka*

6 [m]Kwa hiyo, tukiachana na mafundisho
yale ya awali kuhusu Kristo na tukisonga
mbele ili tufikie utimilifu, sio kuweka tena
msingi wa mafundisho ya kuzitubia kazi
zisizo na uhai na imani katika Mungu,
2 [n]mafundisho kuhusu aina za ubatizo,
kuwekea watu mikono, ufufuo wa wafu,
na hukumu ya milele. 3 [o]Mungu akitujalia
tutafanya hivyo.

4 [p]Kwa kuwa ni vigumu kwa wale
ambao wakati fulani walishapata nuru,
ambao walishaonja kipawa cha mbinguni,
ambao wamekwisha kushiriki katika Roho
Mtakatifu, 5 [q]ambao wameonja uzuri wa
Neno la Mungu na nguvu za wakati ujao,
6 [r]kisha wakianguka, kuwarejesha tena
katika toba. Kwa kuwa wanamsulubisha
Mwana wa Mungu mara ya pili na
kumdhalilisha hadharani, nayo ikawa
hasara kwao.

7 [s]Ardhi ile ipokeayo mvua inyeshayo
juu yake mara kwa mara hutoa mazao
yanayowanufaisha wale ambao kwa ajili
yao yalimwa, nayo nchi hiyo hupokea
baraka kutoka kwa Mungu. 8 [t]Lakini ardhi
ikizaa miiba na mibaruti, haina thamani na
iko hatarini ya kulaaniwa. Mwisho wake ni
kuchomwa moto.

---

[a]**5:3** Law 4:3; 9:7; 16:6; 15:16, 17; Ebr 7:27; 9:7
[b]**5:4** Kut 28:1; Hes 14:40; 18:7; 2Nya 26:18; 1Nya 23:13; Yn 3:27
[c]**5:5** Yn 8:54; Ebr 2:17; 1:5; 1:1; Za 2:7; Mdo 13:33
[d]**5:6** Ebr 5:10; 6:20; 7:2-22; 7:17, 21; Mwa 14:18; Za 110:4
[e]**5:7** Lk 22:41-44; 23:46; Mt 27:46; Za 22:24; Mk 14:36
[f]**5:8** Ebr 1:2; 3:6; Flp 2:8
[g]**5:9** Ebr 2:10; 11:40; Isa 45:17; Yn 17:1, 5
[h]**5:10** Ebr 5:6; 6:20; 2:17
[i]**5:11** Yn 16:12; 2Pet 3:16; Mt 13:15
[j]**5:12** Ebr 6:1; 1Kor 3:2; 1Pet 2:2
[k]**5:13** 1Kor 13:11; 14:20; Efe 4:14; 1Pet 2:2
[l]**5:14** 1Kor 2:6; Isa 7:15; 1Kor 2:14, 15
[m]**6:1** Flp 3:12, 13, 14; Ebr 5:12; 9:14
[n]**6:2** Yn 3:25; Mdo 6:6; 2:24; 17:18, 22
[o]**6:3** Mdo 18:21; 1Kor 4:19
[p]**6:4** Ebr 10:22; Efe 2:8; Gal 3:2; Mt 12:31, 32; 2Pet 2:20, 21; 1Yn 5:16; Yn 4:10; 6:32
[q]**6:5** Ebr 2:5; 4:12; Za 34:8
[r]**6:6** 2Pet 2:21; 1Yn 5:16; Mt 4:3; Ebr 10:29
[s]**6:7** Za 65:10; Mwa 1:11, 12
[t]**6:8** Mwa 3:17, 18; Isa 5:6; 27:4

9 [a]Ingawa tunasema hivi, ndugu zangu
wapendwa, kwa upande wenu tuna hakika
ya mambo mema zaidi, mambo yale
yahusuyo wokovu. 10 [b]Mungu si mdhalimu:
yeye hataisahau kazi yenu na upendo
ule mlioonyesha kwa ajili yake katika
kuwahudumia watakatifu na hata sasa
mnaendelea kuwahudumia. 11 [c]Nasi twataka
kila mmoja wenu aonyeshe bidii iyo hiyo ili
mpate kujua uhakika kamili wa lile tumaini
mpaka mwisho, 12 [d]ili msije mkawa wavivu,
bali mpate kuwaiga wale ambao kwa imani
na saburi hurithi zile ahadi.

*Uhakika Wa Ahadi Ya Mungu*

13 [e]Mungu alipompa Abrahamu ahadi
yake, kwa kuwa hakuwepo mwingine
aliyekuwa mkuu kuliko yeye ambaye
angeweza kuapa kwa jina lake, aliapa
kwa nafsi yake, 14 [f]akisema, "Hakika
nitakubariki na kukupa wazao wengi."
15 [g]Abrahamu naye, baada ya kungoja kwa
saburi, alipokea kile kilichoahidiwa.

16 [h]Wanadamu huapa kwa yeye aliye
mkuu kuwaliko, nacho kiapo hicho
huthibitisha kile kilichosemwa na hivyo
humaliza mabishano yote. 17 [i]Mungu
alipotaka kuonyesha kwa udhahiri zaidi
ile asili ya kutokubadilika kwa ahadi yake
kwa warithi wa ahadi, aliithitibisha kwa
kiapo. 18 [j]Mungu alifanya hivyo ili kwa
vitu viwili visivyobadilika, yaani ahadi
yake na kiapo chake, ambavyo kwavyo
Mungu hawezi kusema uongo, sisi ambao
tumemkimbilia ili tulishike lile tumaini
lililowekwa mbele yetu tuwe na faraja
thabiti. 19 [k]Tunalo tumaini hili kama nanga
ya roho iliyo imara na thabiti. Tumaini hili
huingia katika sehemu takatifu iliyopo
nyuma ya pazia, 20 [l]mahali ambapo Yesu
mtangulizi wetu aliingia kwa niaba yetu.
Yeye amekuwa Kuhani Mkuu milele, kwa
mfano wa Melkizedeki.

[a]**6:9** 1Kor 10:14
[b]**6:10** Mt 10:40, 42; 1The 1:3
[c]**6:11** Ebr 3:6, 14; Kol 2:2; Flp 1:6
[d]**6:12** Ebr 13:7; 10:36; 2The 1:4; Yak 1:3; Ufu 13:10; 14:12
[e]**6:13** Mwa 22:16, 17; Lk 1:73; Za 105:9
[f]**6:14** Mwa 22:17
[g]**6:15** Mwa 21:5
[h]**6:16** Kut 22:10
[i]**6:17** Ebr 6:18; Za 110:4; Rum 4:16; Ebr 11:9; Rum 11:29
[j]**6:18** Hes 23:19; Tit 1:2; Ebr 3:6
[k]**6:19** Law 16:2; Ebr 9:2, 3, 7

*Kuhani Melkizedeki*

7 [m]Kwa kuwa huyu Melkizedeki alikuwa
mfalme wa Salemu na kuhani wa Mungu
Aliye Juu Sana. Alipokutana na Abrahamu
akirudi kutoka kuwashinda hao wafalme,
Melkizedeki alimbariki, 2 naye Abrahamu
alimpa sehemu ya kumi[n] ya kila kitu.
Kwanza, jina hilo Melkizedeki maana
yake ni "mfalme wa haki." Na pia "mfalme
wa Salemu" maana yake ni "mfalme wa
amani." 3 [o]Hana Baba wala mama, hana
ukoo, hana mwanzo wala mwisho wa siku
zake. Kama Mwana wa Mungu, yeye adumu
akiwa kuhani milele.

4 [p]Tazama jinsi alivyokuwa mkuu:
Hata Abrahamu, baba yetu mkuu, alimpa
sehemu ya kumi ya nyara zake. 5 [q]Basi sheria
inawaagiza wana wa Lawi ambao hufanyika
makuhani kupokea sehemu ya kumi kutoka
kwa watu ambao ni ndugu zao, ingawa
ndugu zao ni wazao wa Abrahamu. 6 [r]Huyu
Melkizedeki, ingawa hakufuatia ukoo
wake kutoka kwa Lawi, lakini alipokea
sehemu ya kumi kutoka kwa Abrahamu na
kumbariki yeye aliyekuwa na zile ahadi.
7 Wala hakuna shaka kwamba mdogo
hubarikiwa na aliye mkuu kumliko yeye.
8 [s]Kwa upande mmoja, sehemu ya kumi
hupokelewa na wale ambao hupatikana
na kufa; lakini kwa upande mwingine
hupokelewa na yeye ambaye hushuhudiwa
kuwa yu hai. 9 Mtu anaweza hata kusema
kwamba Lawi, ambaye hupokea sehemu ya
kumi, alitoa hiyo sehemu ya kumi kupitia

[l]**6:20** Ebr 4:14; 2:17; 5:6
[m]**7:1** Za 76:2; Mk 5:7; Ebr 7:6; Mwa 14:18-20
[n]2 Sehemu ya kumi mahali pengine huitwa fungu la kumi au zaka; sehemu ya kumi ya pato hutolewa kwa Mungu.
[o]**7:3** Ebr 7:6; Mt 4:3; Za 110:4
[p]**7:4** Mwa 14:20; Mdo 2:29
[q]**7:5** Hes 18:21, 26
[r]**7:6** Mwa 14:19, 20; Rum 4:13
[s]**7:8** Ebr 5:6; 6:20

kwa Abrahamu, 10 kwa sababu Melkizedeki
alipokutana na Abrahamu, Lawi alikuwa
bado katika viuno vya baba yake wa
zamani.[a]

*Yesu Mfano Wa Melkizedeki*

11 [b]Kama ukamilifu ungeweza kupatikana
kwa njia ya ukuhani wa Walawi (kwa
kuwa katika msingi huo, sheria ilitolewa
kwa watu), kwa nini basi imekuwepo
haja ya kuja kuhani mwingine: kuhani
kwa mfano wa Melkizedeki, wala si kwa
mfano wa Aroni? 12 Kwa kuwa yanapotokea
mabadiliko ya ukuhani, pia lazima yawepo
mabadiliko ya sheria. 13 [c]Yeye ambaye
mambo haya yanasemwa alikuwa wa kabila
lingine, na hakuna mtu wa kabila hilo
aliyewahi kuhudumu katika madhabahu.
14 [d]Kwa maana ni dhahiri kwamba Bwana
wetu alitoka katika uzao wa Yuda, tena
kuhusu kabila hilo Mose hakusema lolote
kwa habari za makuhani. 15 Tena hayo
tuliyosema yako wazi zaidi kama akitokea
kuhani mwingine kama Melkizedeki, 16 yeye
ambaye amefanyika kuhani si kwa misingi
ya sheria kama ilivyokuwa kwa baba zake,
bali kwa misingi ya uwezo wa uzima
usioharibika. 17 [e]Kwa maana imeshuhudiwa
kwamba:

"Wewe ni kuhani milele,
kwa mfano wa Melkizedeki."

18 [f]Kwa upande mmoja, ile amri ya
mwanzo isiyofaa na dhaifu imebatilishwa
19 [g](kwa maana sheria haikufanya kitu
chochote kuwa kikamilifu). Kwa upande
mwingine, tumeletewa tumaini lililo bora
zaidi ambalo linatuleta karibu na Mungu.
20 Nalo tumaini hilo halikutolewa pasipo
kiapo! Wengine walikuwa makuhani
pasipo kiapo chochote, 21 [h]lakini Yesu
alifanywa kuhani kwa kiapo wakati Mungu
alimwambia:

"Bwana ameapa
naye hatabadilisha mawazo yake:
'Wewe ni kuhani milele.' "

22 [i]Kwa ajili ya kiapo hiki, Yesu amekuwa
mdhamini wa agano lililo bora zaidi.
23 Basi pamekuwepo na makuhani wengi
wa aina hiyo, kwa kuwa kifo kiliwazuia
kuendelea na huduma yao ya ukuhani.
24 [j]Lakini kwa sababu Yesu anaishi milele,
anao ukuhani wa kudumu. 25 [k]Kwa hiyo
anaweza kuwaokoa kabisa wale wanaomjia
Mungu kupitia kwake, kwa sababu yeye
adumu daima kuomba kwa ajili yao.
26 [l]Kwa kuwa ilitupasa tuwe na
Kuhani Mkuu wa namna hii, yaani, aliye
mtakatifu, asiye na lawama, asiye na
dosari, aliyetengwa na wenye dhambi na
kuinuliwa juu ya mbingu. 27 [m]Yeye hahitaji
kutoa dhabihu siku kwa siku kwa ajili ya
dhambi, kwanza kwa ajili ya dhambi zake
mwenyewe, kisha kwa ajili ya dhambi za
watu kama wale makuhani wakuu wengine.
Yeye alitoa dhabihu kwa ajili ya dhambi
zao mara moja tu, alipojitoa mwenyewe.
28 [n]Kwa kuwa sheria huwaweka makuhani
wakuu watu ambao ni dhaifu; lakini lile
neno la kiapo, lililokuja baada ya sheria,
lilimweka Mwana, ambaye amefanywa
kuwa mkamilifu milele.

*Kuhani Mkuu Wa Agano Jipya*

8 [o]Basi jambo tunalotaka kulisema ni hili:
Tunaye Kuhani Mkuu ambaye ameketi
mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Aliye

---

[a]10 Yaani, alikuwa hajazaliwa.
[b]**7:11** Ebr 7:18-19; 8:7; 10:1; 7:17; 5:6; Gal 2:21
[c]**7:13** Ebr 7:11, 14
[d]**7:14** Isa 11:1; Mt 1:3; 2:6; Lk 3:33; Ufu 5:5
[e]**7:17** Za 110:4; Ebr 7:21; 5:6, 10; 6:20
[f]**7:18** Rum 8:3; Gal 4:9
[g]**7:19** Ebr 7:11; 9:9; 10:1; Rum 3:20; 7:7, 8; Gal 3:21; Yak 4:8
[h]**7:21** Za 110:4; Hes 23:19; 1Sam 15:29; Mal 3:6; Rum 1:29; Ebr 5:6
[i]**7:22** Ebr 8:6; 9:15; 12:24; Lk 22:20
[j]**7:24** Ebr 7:28
[k]**7:25** Rum 11:14; 8:34; Ebr 7:19; 1Tim 2:5; 1Yn 2:1
[l]**7:26** Ebr 4:15; 8:1; Efe 1:20; 4:10; 2Kor 5:21
[m]**7:27** Ebr 5:1, 3; Rum 6:10; Ebr 9:12, 26, 28; 10:10; 1Pet 3:18; Efe 5:2
[n]**7:28** Ebr 5:2; 1:2; 2:10
[o]**8:1** Ebr 2:17; Mk 16:19; Ebr 4:14; Efe 1:20; Kol 3:1

Mkuu mbinguni, 2 [a]yeye ahudumuye katika
patakatifu, hema la kweli lililowekwa na
Bwana, wala si na mwanadamu.
3 [b]Kila kuhani mkuu huwekwa ili atoe
sadaka na dhabihu. Vivyo hivyo, ilikuwa
jambo muhimu kwa huyu Kuhani naye
awe na kitu cha kutoa. 4 [c]Kama angekuwa
duniani, hangekuwa kuhani, kwa sababu
tayari wapo watu watoao sadaka kama
ilivyoelekezwa na sheria. 5 [d]Wanahudumu
katika patakatifu palipo mfano na kivuli
cha mambo ya mbinguni. Hii ndiyo sababu
Mose alionywa alipokaribia kujenga
hema, akiambiwa: "Hakikisha kuwa
unavitengeneza vitu vyote kwa mfano
ulioonyeshwa kule mlimani." 6 [e]Lakini
huduma aliyopewa Yesu ni bora zaidi
kuliko yao, kama vile agano ambalo yeye
ni mpatanishi wake lilivyo bora zaidi kuliko
lile la zamani, nalo limewekwa misingi wa
ahadi zilizo bora zaidi.
7 [f]Kwa maana kama hapakuwa na kasoro
katika lile agano la kwanza, pasingekuwa
na haja ya kutafuta nafasi kwa ajili ya
jingine. 8 [g]Lakini Mungu aliona kosa kwa
watu, naye akasema:

"Siku zinakuja, asema Bwana,
nitakapofanya agano jipya
na nyumba ya Israeli
na nyumba ya Yuda.
9 [h]Agano langu halitakuwa kama lile
nililofanya na baba zao
nilipowashika mkono
kuwaongoza watoke nchi ya Misri,
kwa sababu hawakuendelea kuwa
waaminifu katika agano
langu,
nami nikawaacha,
asema Bwana.
10 [i]Hili ndilo agano nitakalofanya na
nyumba ya Israeli
baada ya siku zile, asema Bwana.
Nitaziweka sheria zangu katika nia
zao
na kuziandika mioyoni mwao.
Nitakuwa Mungu wao,
nao watakuwa watu wangu.
11 [j]Mtu hatamfundisha tena jirani yake,
wala mtu kumfundisha ndugu
yake akisema, 'Mjue Bwana,'
kwa sababu wote watanijua mimi,
tangu aliye mdogo kabisa kwao,
hadi aliye mkuu sana.
12 [k]Kwa sababu nitasamehe uovu wao,
wala sitazikumbuka dhambi zao
tena!"

13 [l]Kwa kuliita agano hili "jipya," Mungu
amefanya lile agano la kwanza kuwa
kuukuu; nacho kitu kinachoanza kuchakaa
na kuwa kikuukuu kiko karibu kutoweka.

*Ibada Katika Hema La Kidunia*

9 [m]Basi agano lile la kwanza lilikuwa na
kanuni zake za kuabudu na pia patakatifu
pake pa kidunia. 2 [n]Hema ilitengenezwa.
Katika sehemu yake ya kwanza kulikuwa na
kinara cha taa, meza na mikate iliyowekwa
wakfu; hii sehemu iliitwa Mahali Patakatifu.
3 [o]Nyuma ya pazia la pili, palikuwa na
sehemu iliyoitwa Patakatifu pa Patakatifu,
4 [p]ambapo palikuwa na yale madhabahu
ya dhahabu ya kufukizia uvumba, na
lile Sanduku la Agano lililofunikwa kwa
dhahabu. Sanduku hili lilikuwa na gudulia
la dhahabu lenye mana, ile fimbo ya Aroni
iliyochipuka, na vile vibao vya mawe vya

---

[a]**8:2** Ebr 9:11, 24; 9:8, 12, 24
[b]**8:3** Ebr 2:17; 5:1; 9:9, 14; Efe 5:2
[c]**8:4** Ebr 5:1; 9:9
[d]**8:5** Ebr 9:23; 10:1; 11:7; 12:25; Kol 2:17; Kut 25:40
[e]**8:6** Ebr 8:8, 13; Lk 22:20; Gal 3:20; 2Kor 3:6, 8, 9
[f]**8:7** Ebr 7:11, 18; 10:1
[g]**8:8** Yer 31:31, 32, 33, 34; Ebr 10:16, 17
[h]**8:9** Kut 19:5-6; 20:1-17
[i]**8:10** Rum 11:27; 2Kor 3:3; Ebr 10:16; Eze 11:20; Zek 8:8
[j]**8:11** Isa 54:13; Yn 6:45
[k]**8:12** Ebr 10:17; Yer 31:31-34
[l]**8:13** Ebr 8:6, 8; Lk 22:20; 2Kor 5:17; Rum 10:4
[m]**9:1** Kut 25:8
[n]**9:2** Kut 26:1; 26:35; 40:4; 25:31; 25:23; Law 24:5
[o]**9:3** Kut 26:31, 33; 40:3, 21; Ebr 6:19
[p]**9:4** Kut 30:1-5; 25:10-22; 16:32, 33; Hes 17:10; Kut 31:18; 32:15

Agano. 5 [a]Juu ya lile Sanduku kulikuwa na
makerubi ya Utukufu yakitilia kivuli kile
kifuniko ambacho ndicho kiti cha rehema.
Lakini hatuwezi kueleza vitu hivi kwa
undani sasa.

6 [b]Basi vitu hivi vilipokuwa vimepangwa,
makuhani waliingia daima katika sehemu
ya kwanza ya hema ili kufanya taratibu zao
za ibada. 7 [c]Lakini ni kuhani mkuu peke
yake aliyeingia ndani ya sehemu ya pili ya
hema. Tena hii ilikuwa mara moja tu kwa
mwaka, na hakuingia kamwe bila damu,
ambayo alitoa kwa ajili yake mwenyewe na
kwa ajili ya dhambi za watu walizotenda
bila kukusudia. 8 [d]Kwa njia hii, Roho
Mtakatifu alikuwa anaonyesha kwamba,
maadamu ile hema ya kwanza ilikuwa bado
imesimama, njia ya kuingia Patakatifu pa
Patakafifu ilikuwa bado haijafunguliwa.
9 [e]Huu ulikuwa mfano kwa ajili ya wakati
wa sasa, kuonyesha kwamba sadaka na
dhabihu zilizokuwa zikitolewa hazikuweza
kusafisha dhamiri ya mtu anayeabudu.
10 [f]Lakini hizi zilishughulika tu na vyakula
na vinywaji, pamoja na taratibu mbalimbali
za kunawa kwa nje, kanuni kwa ajili ya
mwili zilizowekwa hadi wakati utimie wa
matengenezo mapya.

*Damu Ya Kristo*

11 [g]Kristo alipokuja akiwa Kuhani
Mkuu wa mambo mema ambayo tayari
yameshawasili, alipitia kwenye hema
iliyo kuu zaidi na bora zaidi, ambayo
haikutengenezwa kwa mikono ya
binadamu, hii ni kusema, ambayo si sehemu
ya uumbaji huu. 12 [h]Hakuingia kwa njia ya
damu ya mbuzi na ya ndama; lakini aliingia
Patakatifu pa Patakatifu mara moja tu kwa
damu yake mwenyewe, akiisha kupata
ukombozi wa milele. 13 [i]Damu ya mbuzi
na ya mafahali, na majivu ya mitamba
walivyonyunyiziwa wale waliokuwa najisi
kwa taratibu za kiibada viliwatakasa, hata
kuwaondolea uchafu wa nje. 14 [j]Basi ni zaidi
aje damu ya Kristo, ambaye kwa Roho wa
milele alijitoa nafsi yake kwa Mungu kuwa
sadaka isiyo na waa, itatusafisha dhamiri
zetu kutokana na matendo yaletayo mauti,
ili tupate kumtumikia Mungu aliye hai!

15 [k]Kwa sababu hii Kristo ni mpatanishi
wa agano jipya, ili kwamba wale walioitwa
waweze kupokea ile ahadi ya urithi wa
milele: kwa vile yeye alikufa awe ukombozi
wao kutoka kwa dhambi walizozitenda
chini ya agano la kwanza.

16 Kwa habari ya wosia,[l] ni muhimu
kuthibitisha kifo cha yule aliyeutoa,
17 [m]kwa sababu wosia huwa na nguvu tu
wakati mtu ameshakufa; kamwe hauwezi
kutumika wakati yule aliyeuandika bado
yuko hai. 18 [n]Hii ndiyo sababu hata lile
agano la kwanza halikuweza kutekelezwa
pasipo damu. 19 [o]Mose alipotangaza kila
amri kwa watu wote, alichukua damu ya
ndama na ya mbuzi, pamoja na maji, sufu
nyekundu na matawi ya mti wa hisopo,
akanyunyizia kile kitabu na watu wote.
20 [p]Alisema, "Hii ndiyo damu ya agano,
ambalo Mungu amewaamuru kulitii."
21 [q]Vivyo hivyo alinyunyizia damu hiyo
kwenye ile hema pamoja na kila kifaa
kilichotumika ndani yake kwa taratibu za
ibada. 22 [r]Kwa kweli sheria hudai kwamba,
karibu kila kitu kitakaswe kwa damu, wala

[a]**9:5** Kut 25:17-19; 25:20-22; 26:34
[b]**9:6** Hes 28:3
[c]**9:7** Law 16:11-19; Ebr 9:2, 3; Law 16:34
[d]**9:8** Ebr 3:7; Yn 14:6; Ebr 10:19, 20
[e]**9:9** Ebr 10:1; 5:1; 8:3; 7:19
[f]**9:10** Law 11:2-23; Hes 6:3; Kol 2:16; Law 11:25, 28, 40; Ebr 7:16
[g]**9:11** Ebr 2:17; 10:1; 9:24; 8:2; Yn 2:19
[h]**9:12** Ebr 9:19; Law 16:6, 15; Ebr 10:4; 9:24, 26, 28; Rum 3:25
[i]**9:13** Ebr 10:4; Hes 19:9, 17, 18
[j]**9:14** 1Pet 3:18; Efe 5:2; Za 51:2; 65:3; Yer 33:8; Zek 13:1; Tit 2:14; Mt 16:16
[k]**9:15** Gal 3:20; Lk 22:20; Rum 8:28; 11:29; Ebr 6:15; 7:22; Mdo 20:32
[l]16 Wosia hapa kwa neno la Kiyunani ni agano.
[m]**9:17** Gal 3:15
[n]**9:18** Kut 24:6-8
[o]**9:19** Kut 24:5, 6, 8; Law 16:14, 15, 18; 14:4, 6, 7, 49, 51, 52
[p]**9:20** Kut 24:8; Mt 26; 28
[q]**9:21** Kut 29:12, 36; Law 8:15, 19; 16:1, 15, 16, 18, 19
[r]**9:22** Law 17:11; Kut 29:21; Law 8:15

pasipo kumwaga damu, hakuna msamaha
wa dhambi.
23 [a]Kwa hiyo, ilikuwa muhimu kwa nakala
za vitu vile vya mbinguni vitakaswe kwa
dhabihu hizi, lakini vitu halisi vya mbinguni
vilihitaji dhabihu bora kuliko hizi. 24 [b]Kwa
maana Kristo hakuingia kwenye patakatifu
palipofanywa kwa mikono ya mwanadamu,
ambao ni mfano wa kile kilicho halisi.
Yeye aliingia mbinguni penyewe, ili sasa
aonekane mbele za Mungu kwa ajili yetu.
25 [c]Wala hakuingia mbinguni ili apate
kujitoa mwenyewe mara kwa mara, kama
vile kuhani mkuu aingiavyo Patakatifu pa
Patakatifu kila mwaka kwa damu ambayo
si yake mwenyewe. 26 [d]Ingekuwa hivyo,
ingempasa Kristo kuteswa mara nyingi
tangu kuumbwa kwa ulimwengu. Lakini
sasa ametokea mara moja tu katika mwisho
wa nyakati aiondoe dhambi kwa kujitoa
mwenyewe kuwa dhabihu. 27 [e]Kama vile
mwanadamu alivyowekewa kufa mara
moja tu na baada ya kufa akabili hukumu,
28 [f]vivyo hivyo Kristo alitolewa mara moja
tu kuwa dhabihu ili azichukue dhambi za
watu wengi. Naye atakuja mara ya pili, sio
kuchukua dhambi, bali kuwaletea wokovu
wale wanaomngoja kwa shauku.

*Dhabihu Ya Kristo Ni Mara Moja Tu*

10 [g]Sheria ni kivuli tu cha mambo mema
yajayo, wala si uhalisi wa mambo
yenyewe. Kwa sababu hii, haiwezekani
kamwe kwa njia ya dhabihu zitolewazo
mwaka hadi mwaka kuwakamilisha
wale wanaokaribia ili kuabudu. 2 [h]Kama
dhabihu hizo zingeweza kuwakamilisha,
hazingeendelea kutolewa tena. Kwa kuwa
hao waabuduo wangekuwa wametakaswa
mara moja tu, wala wasingejiona tena kuwa
na dhambi. 3 [i]Lakini zile dhabihu zilikuwa
ukumbusho wa dhambi kila mwaka, 4 [j]kwa
sababu haiwezekani damu ya mafahali na
mbuzi kuondoa dhambi.
5 [k]Kwa hiyo, Kristo alipokuja duniani,
alisema:

“Dhabihu na sadaka hukuzitaka,
bali mwili uliniandalia;
6 sadaka za kuteketezwa na za dhambi
hukupendezwa nazo.
7 [l]Ndipo niliposema, ‘Mimi hapa,
nimekuja,
imeandikwa kunihusu katika
kitabu:
Nimekuja kuyafanya mapenzi yako,
Ee Mungu.’ ”

8 [m]Kwanza alisema, “Dhabihu na sadaka,
sadaka za kuteketezwa na za dhambi
hukuzitaka, wala hukupendezwa nazo”
(ingawa sheria iliagiza zitolewe). 9 [n]Kisha
akasema “Mimi hapa, nimekuja kuyafanya
mapenzi yako.” Aondoa lile Agano la
kwanza ili kuimarisha la pili. 10 [o]Katika
mapenzi hayo sisi tumetakaswa na
kufanywa watakatifu kwa njia ya sadaka
ya mwili wa Yesu Kristo alioutoa mara
moja tu.
11 [p]Kila kuhani husimama siku kwa siku
akifanya huduma yake ya ibada, na kutoa
tena na tena dhabihu zile zile ambazo
haziwezi kamwe kuondoa dhambi. 12 [q]Lakini
huyu kuhani akiisha kutoa dhabihu moja
kwa ajili ya dhambi kwa wakati wote,
aliketi mkono wa kuume wa Mungu.
13 [r]Tangu wakati huo anangoja mpaka

[a]**9:23** Ebr 8:5
[b]**9:24** Ebr 6:20; 8:2; Rum 8:34; Ebr 7:25; 1Yn 2:1
[c]**9:25** Ebr 9:7; 10:19
[d]**9:26** Ebr 9:12; 7:27; 10:10; 1Pet 3:18; 1Kor 10:11; Gal 4:4; Efe 1:10
[e]**9:27** Mwa 3:19; Mhu 3:20; 2Kor 5:10; Ufu 20:12, 13
[f]**9:28** Rum 6:10; 1Pet 3:18; 2:24; 1Yn 3:5; Mt 26:28; Rum 5:15; Tit 2:13
[g]**10:1** Kol 2:17; Ebr 8:5; 9:23; 9:11; 9:9; 9:14
[h]**10:2** Ebr 9:9
[i]**10:3** Law 16:21; 16:34; Ebr 9:7
[j]**10:4** Mik 6:6, 7; Ebr 9:13; 9:11
[k]**10:5** Ebr 1:6; 2:14; 1Pet 2:24; Za 40:6; 50:8; Isa 1:11; Yer 6:20; Amo 5:21, 22
[l]**10:7** Ezr 6:2; Yer 36:2; Za 40:6-8; Mt 26:39
[m]**10:8** Ebr 10:5, 6; Mk 12:33
[n]**10:9** Ebr 10:7
[o]**10:10** Ebr 10:14; Efe 5:26; Ebr 2:14; 7:27; 1Pet 2:24
[p]**10:11** Ebr 5:1; 10:1, 4; Hes 28:3; Ebr 7:27
[q]**10:12** Ebr 5:1; Mk 16:19; Ebr 1:3; Kol 3:1
[r]**10:13** Yos 10:24; Ebr 1:13; Za 110:1; Mdo 2:35; 1Kor 15:25

adui zake wawekwe chini ya miguu
yake, 14 [a]kwa sababu kwa dhabihu moja
amewafanya kuwa wakamilifu milele wale
wote wanaotakaswa.
15 [b]Pia Roho Mtakatifu anatushuhudia
kuhusu jambo hili. Kwanza anasema:

16 [c]“Hili ndilo Agano nitakalofanya nao
baada ya siku hizo, asema Bwana.
Nitaziweka sheria zangu mioyoni
mwao,
na kuziandika katika nia zao.”

17 [d]Kisha aongeza kusema:

“Dhambi zao na kutokutii kwao
sitakumbuka tena.”

18 Basi haya yakiisha kusamehewa, hakuna
tena dhabihu yoyote inayotolewa kwa ajili
ya dhambi.

*Wito Wa Kuvumilia*

19 [e]Kwa hiyo, ndugu zangu, kwa kuwa
tunao ujasiri wa kupaingia Patakatifu pa
Patakatifu kwa damu ya Yesu, 20 [f]kwa
njia mpya iliyo hai tuliyofunguliwa kwa
ajili yetu kupitia kwenye lile pazia, yaani,
mwili wake, 21 [g]basi kwa kuwa tunaye
Kuhani Mkuu juu ya nyumba ya Mungu,
22 [h]sisi na tumkaribie Mungu kwa moyo
mnyofu kwa imani timilifu, mioyo yetu
ikiwa imenyunyizwa damu ya Kristo na
kuwa safi kutokana na dhamiri mbaya nayo
miili yetu ikiwa imeoshwa kwa maji safi.
23 [i]Tushike kwa uthabiti lile tumaini la ukiri
wetu bila kuyumbayumba, kwa maana yeye
aliyeahidi ni mwaminifu. 24 [j]Tuangaliane
na kuhimizana sisi kwa sisi katika upendo
na katika kutenda mema. 25 [k]Wala tusiache
kukutana pamoja, kama wengine walivyo
na desturi, bali tuhimizane sisi kwa sisi
kadiri tuonavyo Siku ile inakaribia.
26 [l]Kama tukiendelea kutenda dhambi
kwa makusudi baada ya kupokea ufahamu
wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa
ajili ya dhambi. 27 [m]Lakini kinachobaki
ni kungoja kwa hofu hukumu ya moto
uwakao, utakaowaangamiza adui za Mungu.
28 [n]Yeyote aliyeikataa sheria ya Mose
alikufa pasipo huruma kwa ushahidi wa
watu wawili au watatu. 29 [o]Je, mnadhani ni
adhabu kali kiasi gani anayostahili kupewa
mtu aliyemkanyaga Mwana wa Mungu
chini ya nyayo zake, yeye aliyeifanya damu
ya Agano iliyomtakasa kuwa kitu najisi na
kumtendea maovu Roho wa neema? 30 [p]Kwa
kuwa tunamjua yeye aliyesema, “Ni juu
yangu kulipiza kisasi; nitalipiza.” Tena
asema, “Bwana atawahukumu watu wake.”
31 [q]Ni jambo la kutisha kuanguka mikononi
mwa Mungu aliye hai.
32 [r]Kumbukeni siku zile za kwanza,
ambazo mkiisha kutiwa nuru mlistahimili
mashindano makali ya maumivu. 33 Wakati
mwingine mlitukanwa na kuteswa
hadharani; wakati mwingine mlikuwa
radhi kuungana na wale waliofanyiwa
hivyo. 34 [s]Mliwahurumia wale waliokuwa
kifungoni, mkikubali kwa furaha
kunyang’anywa mali zenu kwa maana
mlijua kwamba mnayo mali iliyo bora zaidi
idumuyo.
35 [t]Kwa hiyo msiutupe ujasiri wenu,
kwa maana una thawabu kubwa mno.

---

[a]**10:14** Ebr 10:1; Efe 5:26
[b]**10:15** Ebr 3:7
[c]**10:16** Yer 31:33; Ebr 8:10
[d]**10:17** Yer 31:34; Ebr 8:12
[e]**10:19** Efe 3:12; Law 16:2; Efe 2:18; Ebr 9:8, 12, 25
[f]**10:20** Ebr 9:8; 6:19; 9:3
[g]**10:21** Ebr 2:17; 3:6
[h]**10:22** Ebr 10:1; 7:19; 3:12; Yak 1:6; 1Yn 3:21; Eze 36:25; 2Kor 7:1; 1Pet 1:2; Mdo 22:16
[i]**10:23** Ebr 3:6; 3; 1; 1Kor 1:9
[j]**10:24** Tit 2:14
[k]**10:25** Mdo 2:42; Ebr 3:13; 1Kor 3:13
[l]**10:26** Kut 21:14; Hes 15:30; Ebr 5:2; 6:4-8; 2Pet 2:20; 1Tim 2:4
[m]**10:27** Isa 26:11; 2The 1:7; Ebr 9:27; 12:29
[n]**10:28** Kum 17:6, 7; Mt 18:16; Ebr 2:2; Yn 8:17
[o]**10:29** Ebr 2:3; 12:25; 1Kor 11:29; Mt 12:32; Efe 4:30; Mt 4:3; Ufu 1:5; Ebr 6:6; Mt 26:28
[p]**10:30** Kum 32:35; Rum 12:19; Kum 32:36; Za 135:14
[q]**10:31** 2Kor 5:11; Isa 19:16; Mt 16:16
[r]**10:32** Ebr 6:4; Flp 1:9, 30; Gal 3:4; 2Yn 8; Kol 2:1
[s]**10:34** Ebr 13:3; 11:16; 1Pet 1:4, 5
[t]**10:35** Efe 3:12; Mt 5:12; 10:32

36 [a]Inawapasa kuvumilia ili mkiisha kufanya
mapenzi ya Mungu mpate kile alichoahidi.
37 [b]Kwa kuwa bado kitambo kidogo tu,

“Yeye ajaye atakuja wala hatakawia.
38 [c]Lakini mwenye haki wangu
ataishi kwa imani.
Naye kama akisitasita,
sina furaha naye.”

39 [d]Lakini sisi hatumo miongoni mwa hao
wanaositasita na kuangamia, bali tuko
miongoni mwa hao wenye imani na hivyo
tunaokolewa.

*Maana Ya Imani*

11 [e]Basi imani ni kuwa na hakika ya
mambo yatarajiwayo, na udhahiri wa
mambo yasiyoonekana. 2 [f]Maana baba zetu
wa kale walipongezwa kwa haya.
3 [g]Kwa imani tunafahamu kwamba
ulimwengu uliumbwa kwa neno la Mungu,
vitu vyote vinavyoonekana havikuumbwa
kutoka kwa vitu vinavyoonekana.

*Mfano Wa Abeli, Enoki Na Noa*

4 [h]Kwa imani Abeli alimtolea Mungu
dhabihu bora zaidi kuliko Kaini. Kwa imani
alishuhudiwa kuwa mwenye haki, Mungu
mwenyewe akazishuhudia sadaka zake.
Kwa imani bado ananena ingawa amekufa.
5 [i]Kwa imani Enoki alitwaliwa kutoka
maisha haya, kiasi kwamba hakuonja mauti.
Hakuonekana, kwa sababu Mungu alikuwa
amemchukua. Kwa kuwa kabla hajatwaliwa
alikuwa ameshuhudiwa kuwa ni mtu
aliyempendeza Mungu. 6 [j]Lakini pasipo
imani haiwezekani kumpendeza Mungu,
kwa maana yeyote anayemjia Mungu
lazima aamini kwamba yeye yuko na ya
kuwa huwapa thawabu wale wamtafutao
kwa bidii.
7 [k]Kwa imani, Noa alipoonywa na Mungu
kuhusu mambo ambayo hayajaonekana
bado, kwa kumcha Mungu alitengeneza
safina ili kuokoa jamaa yake. Kwa imani
yake aliuhukumu ulimwengu na akawa
mrithi wa haki ipatikanayo kwa imani.

*Imani Ya Abrahamu*

8 [l]Kwa imani Abrahamu, alipoitwa aende
mahali ambapo Mungu angempa baadaye
kuwa urithi, alitii na akaenda, ingawa
hakujua anakokwenda. 9 [m]Kwa imani
alifanya maskani yake katika nchi ya ahadi
kama mgeni katika nchi ya kigeni; aliishi
katika mahema, kama Isaki na Yakobo
walivyofanya, waliokuwa pia warithi
pamoja naye wa ahadi ile ile. 10 [n]Kwa maana
alikuwa akiutazamia mji wenye misingi
ya kudumu ambao mwenye kuubuni na
kuujenga ni Mungu.
11 [o]Kwa imani Abrahamu, ingawa alikuwa
mzee wa umri, naye Sara mwenyewe
aliyekuwa tasa, alipokea uwezo wa kuwa
baba kwa sababu alimhesabu Mungu
aliyemwahidi kuwa mwaminifu na kwamba
angetimiza ahadi yake. 12 [p]Hivyo kutokana
na huyu huyu ambaye alikuwa sawa na
mfu, wakazaliwa wazao wengi kama nyota
za mbinguni na kama mchanga wa pwani
usiohesabika.
13 [q]Watu hawa wote wakafa katika imani
bila kuzipokea zile ahadi, lakini waliziona
kwa mbali na kuzishangilia. Nao walikubali
kwamba walikuwa wageni na wasiokuwa
na maskani hapa duniani. 14 [r]Watu wasemao

[a]**10:36** Rum 5:3; Ebr 5:11; 12:1; Yak 1:3, 4, 12; 2Pet 1:6; Ebr 6:15; 9:15
[b]**10:37** Mt 11:3; Ufu 22:20; Lk 18:8; 2Pet 3:9; Hab 2:3, 4
[c]**10:38** Rum 1:17; Gal 3:11; Hab 2:3, 4
[d]**10:39** 2Pet 2:20, 21; Mdo 16:30, 31; 1The 5:9; 2The 2:14
[e]**11:1** Ebr 3:6; 2Kor 4:18; Rum 8:24, 25; 2Kor 4:18; 5:7
[f]**11:2** Ebr 11:4, 39
[g]**11:3** Mwa 1:1; Yn 1:3; Ebr 1:2; 2Pet 3:5
[h]**11:4** Ebr 11:2, 39; Mwa 4:4; 1Yn 3:12; Ebr 12:24
[i]**11:5** Mwa 5:2, 24
[j]**11:6** Ebr 7:19, 25; 10:35
[k]**11:7** Mwa 6:8, 9; 7:1; Rum 3:22, 24; 4:20
[l]**11:8** Mwa 12:7; 12:1-4; Mdo 7:2-4
[m]**11:9** Mwa 23:4; 26:3; 35:12; Ebr 6:17
[n]**11:10** Ebr 12:22; 13:14; Ufu 21:2, 14; Ebr 11:16
[o]**11:11** Mwa 17:17-19; 22:17; 32:12
[p]**11:12** Rum 4:19; Mwa 22:17; 32:12
[q]**11:13** Ebr 11:39; Mt 13:17; Mwa 23:4; Law 25:23; Flp 3:20; 1Pet 1:17
[r]**11:14** Ebr 13:14

mambo kama haya, wanaonyesha wazi
kwamba wanatafuta nchi yao wenyewe.
15 [a]Kwa kweli kama wangekuwa wanafikiri
kuhusu nchi waliyoiacha, wangalipata
nafasi ya kurudi huko. 16 [b]Lakini badala
yake walitamani nchi iliyo bora zaidi,
yaani nchi ya mbinguni. Kwa hiyo Mungu
haoni aibu kuitwa Mungu wao, kwa kuwa
amekwisha kuandaa mji kwa ajili yao.

17 [c]Kwa imani Abrahamu, alipojaribiwa
na Mungu, alimtoa Isaki kuwa dhabihu.
Yeye aliyekuwa amezipokea ahadi za
Mungu alikuwa tayari kumtoa mwanawe,
aliyekuwa mwanawe pekee awe dhabihu.
18 [d]Ingawa Mungu alikuwa amemwambia
Abrahamu, "Uzao wako utahesabiwa
kupitia kwa Isaki," 19 [e]Abrahamu alihesabu
kuwa Mungu angaliweza kumfufua Isaki
kutoka kwa wafu. Na kwa kusema kwa
mfano, alimpata tena Isaki kutoka kwa
wafu.

20 [f]Kwa imani Isaki alimbariki Yakobo
na Esau kuhusu maisha yao ya baadaye.

21 [g]Kwa imani Yakobo alipokuwa anakufa,
alimbariki kila mmoja wa mtoto wa Yosefu,
akamwabudu Mungu akiwa ameegemea juu
ya kichwa cha fimbo yake.

22 [h]Kwa imani, Yosefu alipokaribia
mwisho wa maisha yake, alinena habari
za kutoka kwa wana wa Israeli huko Misri
na akatoa maagizo kuhusu mifupa yake.

*Imani Ya Mose*

23 [i]Kwa imani, wazazi wa Mose walimficha
kwa miezi mitatu baada ya kuzaliwa, kwa
sababu waliona kuwa si mtoto wa kawaida,
wala hawakuiogopa amri ya mfalme.

24 [j]Kwa imani, Mose alipokuwa mtu
mzima, alikataa kuitwa mwana wa binti
Farao. 25 [k]Akachagua kupata mateso pamoja
na watu wa Mungu kuliko kujifurahisha
kwa anasa za dhambi kwa kitambo kidogo
tu. 26 [l]Aliona kushutumiwa kwa ajili ya
Kristo ni utajiri mkubwa zaidi kuliko hazina
za Misri, maana alikuwa anatazamia kupata
thawabu baadaye. 27 [m]Kwa imani Mose
aliondoka Misri bila kuogopa ghadhabu ya
mfalme. Alivumilia kwa sababu alimwona
yeye asiyeonekana kwa macho. 28 [n]Kwa
imani akaadhimisha Pasaka na kunyunyiza
damu, ili yule mwenye kuwaangamiza
wazaliwa wa kwanza asiwaguse wazaliwa
wa Israeli.

*Imani Ya Mashujaa Wengine Wa Israeli*

29 [o]Kwa imani, watu walivuka Bahari ya
Shamu[p] kama vile juu ya nchi kavu; lakini
Wamisri walipojaribu kufanya hivyo,
walitoswa ndani ya maji.

30 [q]Kwa imani kuta za Yeriko zilianguka,
baada ya watu kuzizunguka kwa siku saba.

31 [r]Kwa imani, Rahabu, yule kahaba,
hakuangamizwa pamoja na wale waliomwasi
Mungu, kwa kuwa aliwakaribisha wale
wapelelezi.

32 [s]Basi niseme nini zaidi? Sina wakati wa
kusema habari za Gideoni, Baraka, Samsoni,
Yeftha, Daudi, Samweli na manabii,
33 [t]ambao kwa imani walishinda milki za
wafalme, walitekeleza haki, na wakapokea
ahadi za Mungu; walifunga vinywa vya
simba, 34 [u]wakazima makali ya miali ya moto,
na wakaepuka kuuawa kwa upanga; udhaifu
wao uligeuka kuwa nguvu; pia walikuwa
hodari vitani na kuyafukuza majeshi ya

[a]**11:15** Mwa 24:6-8
[b]**11:16** 2Tim 4:18; Mk 8:38; Mwa 26:24; 28:13; Kut 3:6, 15; Ebr 11:10; 13:14
[c]**11:17** Mwa 22:2-10; Yak 2:21
[d]**11:18** Mwa 21:12; Rum 9:7
[e]**11:19** Rum 4:21; Yn 5:21
[f]**11:20** Mwa 27:27-29
[g]**11:21** Mwa 48:1; 8:22; 47:31
[h]**11:22** Mwa 50:24, 25; Kut 13:19; Yos 24:32
[i]**11:23** Kut 2:2; 1:16, 22; Mdo 7:20
[j]**11:24** Kut 2:10, 11
[k]**11:25** Ebr 11:37; Za 84:10
[l]**11:26** Ebr 13:13; Lk 14:33; Ebr 10:35
[m]**11:27** Kut 12:50-51; 10:28-29; 12:37; 13:17; Ebr 11:18
[n]**11:28** Kut 12:21; 1Kor 10:10
[o]**11:29** Kut 14:21-31; 14:22
[p]29 Yaani Bahari ya Mafunjo.
[q]**11:30** Yos 6:20; 6:12-19
[r]**11:31** Yos 2:1; 9; 14; 6:22-25; Yak 2:25
[s]**11:32** Amu 6:8; 4:5; 13:16; 1Sam 16:1, 13; 1:20
[t]**11:33** 2Sam 8:1-3; Dan 6:22
[u]**11:34** Dan 3:19-27; Kut 18:4; 2Fal 20:7; Amu 15:8

wageni. 35 [a]Wanawake walipokea watu
wao waliokuwa wamekufa, wakafufuliwa.
Lakini wengine waliteswa, nao wakakataa
kufunguliwa, ili wapate ufufuo ulio bora
zaidi. 36 Wengine walidhihakiwa na
kupigwa, hata walifungwa minyororo
na kutiwa gerezani. 37 [b]Walipigwa kwa
mawe; walipasuliwa vipande viwili
kwa msumeno; waliuawa kwa upanga.
Walizungukazunguka wakiwa wamevaa
ngozi za kondoo na mbuzi, wakiwa maskini,
wakiteswa na kutendwa mabaya, 38 [c]watu
ambao ulimwengu haukustahili kuwa nao.
Walizunguka majangwani na milimani,
katika mapango na katika mahandaki
ardhini.
39 [d]Hawa wote walishuhudiwa vyema kwa
sababu ya imani yao, lakini hakuna hata
mmoja wao aliyepokea yale yaliyoahidiwa.
40 [e]Kwa kuwa Mungu alikuwa ametangulia
kutuwekea kitu kilicho bora zaidi ili wao
wasikamilishwe pasipo sisi.

*Mungu Huwaadibisha Wanawe*

12 [f]Kwa sababu hii, kwa kuwa
tumezungukwa na wingu kubwa
namna hii la mashahidi, basi na tuweke
kando kila kitu kinachotuzuia na ile dhambi
inayotuzinga kwa urahisi, nasi tupige
mbio kwa saburi katika yale mashindano
yaliyowekwa kwa ajili yetu. 2 [g]Basi na
tumtazame sana Yesu mwanzilishi na
mkamilishaji wa imani yetu, yeye ambaye
kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake
alistahimili msalaba, bila kujali aibu ya huo
msalaba, naye ameketi mkono wa kuume
wa kiti cha enzi cha Mungu. 3 [h]Mtafakarini
sana yeye aliyestahimili upinzani mkuu
namna hii kutoka kwa watu wenye dhambi,
ili kwamba msije mkachoka na kukata
tamaa.
4 [i]Katika kushindana kwenu dhidi ya
dhambi, bado hamjapigana kiasi cha
kumwaga damu yenu. 5 [j]Nanyi mmesahau
yale maneno ya kuwaonya yanayowataja
ninyi kuwa wana, yakisema:

"Mwanangu, usidharau adhabu ya
Bwana,
wala usikate tamaa akikukemea,
6 [k]kwa sababu Bwana huwaadibisha
wale awapendao,
na humwadhibu kila mmoja
anayemkubali kuwa mwana."

7 [l]Vumilieni taabu kwa ajili ya kufunzwa
adabu. Mungu anawatendea ninyi kama
watoto wake, kwa maana ni mtoto
yupi asiyeadibishwa na mzazi wake?
8 [m]Kama hakuna kuadibishwa (ambalo
ni fungu la watoto wote), basi ninyi ni
watoto wa haramu wala si watoto halali.
9 [n]Tena, sisi sote tunao baba wa kimwili,
waliotuadibisha nasi tukawaheshimu kwa
ajili ya hilo. Je, si inatupasa kujinyenyekeza
zaidi kwa Baba wa roho zetu ili tuishi?
10 [o]Baba zetu walituadibisha kwa kitambo
kidogo kama wao wenyewe walivyoona
vyema, lakini Mungu hutuadibisha kwa
faida yetu ili tupate kushiriki utakatifu
wake. 11 [p]Kuadibishwa wakati wowote
hakuonekani kuwa kitu cha kufurahisha
bali chenye maumivu kinapotekelezwa.
Lakini baadaye huzaa matunda ya haki na
amani kwa wale waliofunzwa nayo.
12 [q]Kwa hiyo, itieni nguvu mikono yenu
iliyo dhaifu na magoti yenu yaliyolegea.
13 [r]Sawazisheni mapito ya miguu yenu,
ili kitu kilicho kiwete kisidhoofishwe bali
kiponywe.

[a]**11:35** 1Fal 17:22, 23; 2Fal 4:36, 37
[b]**11:37** 2Nya 24:21; 1Fal 19:10; Yer 26:23; 2Fal 1:8
[c]**11:38** 1Fal 18:4; 19:9
[d]**11:39** Ebr 11:2, 4, 13; 10:36
[e]**11:40** Ufu 6:11; Ebr 2:10
[f]**12:1** 1Kor 9:24; Ebr 10:36
[g]**12:2** Za 25:15; Ebr 2:10; Flp 2:8, 9; Ebr 13:13; Mk 16:19
[h]**12:3** Gal 6:9; Ufu 2:3
[i]**12:4** Ebr 10:32-34; 13:13
[j]**12:5** Ebr 12:3; Mit 3:11, 12
[k]**12:6** Za 94:12; 119:75; Ufu 3:19; Mit 3:11, 12
[l]**12:7** Kum 8:5; 2Sam 7:14; Mit 13:24
[m]**12:8** 1Pet 5:9
[n]**12:9** Hes 16:22; 27:16; Ufu 22:6; Isa 38:16
[o]**12:10** 2Pet 1:4
[p]**12:11** Isa 32:17; Yak 3:17, 18
[q]**12:12** Isa 35:3
[r]**12:13** Mit 4:26; Gal 6:1

*Onyo Dhidi Ya Kuikataa Neema Ya Mungu*

14 [a]Tafuteni kwa bidii kuwa na amani na
watu wote na huo utakatifu, ambao bila
kuwa nao hakuna mtu atakayemwona
Bwana. 15 [b]Angalieni sana mtu yeyote
asiikose neema ya Mungu na kwamba
shina la uchungu lisije likachipuka na
kuwasumbua na watu wengi wakatiwa
unajisi kwa hilo. 16 [c]Angalieni miongoni
mwenu asiwepo mwasherati au mtu
asiyemcha Mungu kama Esau, ambaye
kwa ajili ya mlo mmoja aliuza haki ya
uzaliwa wake wa kwanza. 17 [d]Baadaye
kama mnavyofahamu, alipotaka kurithi ile
baraka, alikataliwa, maana hakupata nafasi
ya kutubu, ingawa aliitafuta kwa machozi.

18 [e]Hamjaufikia mlima ule uwezao
kuguswa na ambao unawaka moto;
wala kwenye giza, utusitusi na dhoruba;
19 [f]kwenye mlio wa tarumbeta, au kwenye
sauti isemayo maneno ya kutisha kiasi
ambacho wale walioisikia waliomba
wasiambiwe neno jingine zaidi, 20 [g]kwa
sababu hawangeweza kustahimili neno
lile lililoamriwa: "Hata kama mnyama
atagusa mlima huu, atapigwa mawe."
21 [h]Waliyoyaona yalikuwa ya kutisha kiasi
kwamba Mose alisema, "Ninatetemeka kwa
hofu."

22 [i]Lakini ninyi mmekuja Mlima Sayuni,
Yerusalemu ya mbinguni, mji wa Mungu
aliye hai. Mmekuja penye kusanyiko
kubwa la malaika maelfu kwa maelfu
wasiohesabika wanaoshangilia, 23 kwenye
kanisa la wazaliwa wa kwanza wa
Mungu, ambao majina yao yameandikwa
mbinguni. Mmekuja kwa Mungu, mhukumu
wa watu wote, kwenye roho za wenye
haki waliokamilishwa, 24 [j]kwa Yesu
mpatanishi wa agano jipya, na kwa damu
iliyonyunyizwa, ile inenayo mambo mema
kuliko damu ya Abeli.

25 [k]Angalieni, msije mkamkataa yeye
anenaye. Ikiwa wao hawakuepuka adhabu
walipomkataa yeye aliyewaonya hapa
duniani, sisi je, tutaokokaje tusipomsikiliza
yeye anayetuonya kutoka mbinguni?
26 [l]Wakati ule sauti yake ilitetemesha dunia,
lakini sasa ameahidi, "Kwa mara moja tena
nitatetemesha si nchi tu bali na mbingu
pia."

27 [m]Maneno haya "kwa mara moja tena"
yanaonyesha kuondoshwa kwa vile vitu
vinavyoweza kutetemeshwa, yaani vile
vitu vilivyoumbwa, kwa kusudi vile tu
visivyoweza kutetemeshwa vibaki.

28 [n]Kwa hiyo, kwa kuwa tunapokea
ufalme ambao hauwezi kutetemeshwa, basi
na tuwe na shukrani, na hivyo tumwabudu
Mungu kwa namna inayompendeza, kwa
unyenyekevu na uchaji, 29 [o]kwa kuwa
"Mungu wetu ni moto ulao."

*Huduma Inayompendeza Mungu*

13 [p]Endeleeni kupendana kama ndugu.
2 [q]Msisahau kuwakaribisha wageni,
kwa kuwa kwa kufanya hivyo, watu
wengine waliwakaribisha malaika pasipo
kujua. 3 [r]Wakumbukeni wale waliofungwa
gerezani kana kwamba ninyi mmefungwa
pamoja nao. Pia wakumbukeni wale

---

[a]**12:14** Rum 14:19; 6:22; Mt 5:8
[b]**12:15** Gal 5:4; Ebr 3:12; 4:1; Kum 29:18
[c]**12:16** 1Kor 6:18
[d]**12:17** Mwa 27:30-40
[e]**12:18** Kut 19:12-22; 20:18; Kum 4:11
[f]**12:19** Kut 20:18; Kum 4:12; Kut 20:19; Kum 5:5, 25; 18:16
[g]**12:20** Kut 19:12, 13
[h]**12:21** Kum 9:19
[i]**12:22** Isa 24:23; 60:14; Ufu 14:1; Gal 4:26; Ebr 11:10; 13:14; Mit 16:16
[j]**12:24** Gal 3:20; Ebr 9:19; 10:22; 1Pet 1:2; Mwa 4:10; Ebr 11:4
[k]**12:25** Ebr 3:12; 1:1; 8:5; 11:7; 2:2, 3; 10:29; Kum 18:19
[l]**12:26** Kut 19:18; Hag 2:6
[m]**12:27** Isa 34:4; 54:10; 1Kor 7:31; Ebr 1:11; 2Pet 3:10; 1Yn 2:17
[n]**12:28** Za 15:5; Dan 2:44; Mal 2:5; 4:2; Ebr 13:15
[o]**12:29** Kut 24:17; Kum 4:24; 9:3; Za 97:3; Isa 33:14; 1The 1:7
[p]**13:1** Rum 12:10; 1The 4:9; 1Pet 1:22; 2:17; 3:8; 4:8; 2Pet 1:7; 1Yn 3:11; 4:7
[q]**13:2** Mt 25:35; Rum 12:13; 1Tim 3:2; 1Pet 4:9; Mwa 18:3; 19:2
[r]**13:3** Mt 25:36; Kol 4:18; Ebr 10:34; Rum 12:15; 1Kor 12:26; 1Pet 3:8

wanaotendewa vibaya, kana kwamba ni
ninyi wenyewe mnateswa.
4 [a]Ndoa na iheshimiwe na watu wote,
nayo malazi yawe safi, kwa kuwa Mungu
atawahukumu wazinzi na waasherati wote.
5 [b]Yalindeni maisha yenu msiwe na tabia ya
kupenda fedha, bali mridhike na vile mlivyo
navyo, kwa sababu Mungu amesema,

“Kamwe sitakuacha,
wala sitakupungukia.”

6 [c]Kwa hiyo tunaweza kusema kwa ujasiri,

“Bwana ni msaada wangu; sitaogopa.
Mwanadamu anaweza kunitenda
nini?”

7 [d]Wakumbukeni viongozi wenu, wale
waliowaambia neno la Mungu. Angalieni
matokeo ya mwenendo wa maisha yao
mkaiige imani yao. 8 [e]Yesu Kristo ni yeye
yule jana, leo na hata milele.
9 [f]Msichukuliwe na kila aina ya
mafundisho ya kigeni. Ni vyema mioyo yenu
iimarishwe kwa neema, wala si kwa sheria
kuhusu utaratibu wa vyakula, ambavyo
havina faida kwa wale wanaozishika hizo
sheria. 10 [g]Sisi tunayo madhabahu ambayo
wale wanaohudumu katika hema hawana
haki ya kula vile vitu vilivyowekwa juu
yake.
11 [h]Kuhani mkuu huchukua damu ya
wanyama na kuiingiza Patakatifu pa
Patakatifu, kama sadaka ya dhambi, lakini
miili ya hao wanyama huteketezwa nje ya
kambi. 12 [i]Vivyo hivyo, Yesu naye aliteswa
nje ya lango la mji ili awatakase watu kwa
damu yake mwenyewe. 13 [j]Kwa hiyo, basi
na tumwendee nje ya kambi, tukiichukua
aibu aliyobeba. 14 [k]Kwa kuwa hapa hatuna
mji udumuo, bali tunautafuta ule ujao.
15 [l]Basi kwa njia ya Yesu, tuzidi kumtolea
Mungu dhabihu ya sifa, yaani matunda
ya midomo inayolikiri Jina lake. 16 [m]Na
msiache kutenda mema na kushirikiana
vile vitu mlivyo navyo, kwa kuwa dhabihu
kama hizo ndizo zinazompendeza Mungu.
17 [n]Watiini viongozi wenu na
kujinyenyekeza chini ya mamlaka yao. Kwa
maana wao wanakesha kwa ajili yenu kama
watu watakaopaswa kutoa hesabu. Watiini
ili wafanye kazi yao kwa furaha, wala si
kama mzigo, maana hiyo haitakuwa na
faida kwenu.
18 [o]Tuombeeni. Tuna hakika kuwa tunayo
dhamiri safi na shauku ya kuishi kwa
uadilifu kwa kila njia. 19 Ninawasihi zaidi
mniombee ili nipate kurudishwa kwenu
upesi.

### *Maombi Ya Kuwatakia Baraka*

20 Basi Mungu wa amani, ambaye kwa
damu ya Agano la milele alimleta tena
kutoka kwa wafu Bwana wetu Yesu, yule
Mchungaji Mkuu wa kondoo, 21 awafanye
ninyi wakamilifu mkiwa mmekamilishwa
katika kila jambo jema ili mpate kutenda
mapenzi yake, naye atende ndani yetu kile
kinachompendeza machoni Pake, kwa njia
ya Yesu Kristo, ambaye utukufu una yeye
milele na milele. Amen.

### *Maneno Ya Mwisho Na Salamu*

22 [p]Ndugu zangu, nawasihi mchukuliane

---

[a]**13:4** Mal 2:15; 1Kor 7:38; 1Tim 4:3; Kum 22:22; 1Kor 6:9; Efe 5:5; Ufu 22:15
[b]**13:5** 1Tim 3:3; Flp 4:11; Kum 31:6, 8; Yos 1:5; Mwa 28:15; Mt 6:25, 34; 1Nya 28:20; Za 37:25
[c]**13:6** Za 27:1; 56:4; 118:6
[d]**13:7** Ebr 13:17, 24; 1Kor 16:16; Ebr 4:12; 6:12
[e]**13:8** Yn 8:58; Ebr 1:12; Za 102:27; Ufu 1:4
[f]**13:9** Efe 4:14; Kol 2:7; 2:16; Ebr 9:10; Rum 14:17; 1Yn 4:1; 1Tim 4:3
[g]**13:10** 1Kor 9:13; 10:18
[h]**13:11** Law 16:15; Kut 29:14; Law 4:12; 9:11; 16:27; Hes 19:3
[i]**13:12** Yn 19:17, 18; Mdo 7:58; Efe 5:26; Rum 3:25
[j]**13:13** Lk 9:23; Ebr 11:26; 1Pet 4:14
[k]**13:14** Mik 2:10; Flp 3:20
[l]**13:15** 1Pet 2:5; Isa 57:19; Hos 14:2; Efe 5:20; Law 7:12; Za 50:14, 23; 107:22; 116:17; Hos 14:2
[m]**13:16** Rum 12:13; Flp 4:18; 1Kor 9:12; Ebr 6:10
[n]**13:17** Isa 62:6; Mdo 20:28; Ebr 13:7, 24; Flp 2:29; 1The 5:12; 1Tim 5:17; Eze 3:17; 33:2, 7; Mdo 20:26
[o]**13:18** 1The 5:25; Mdo 23:1
[p]**13:22** 1Pet 5:12; Yak 1:21

na maneno yangu ya maonyo, kwa kuwa
nimewaandikia waraka mfupi tu.
23 [a]Nataka ninyi mjue kwamba ndugu yetu
Timotheo amefunguliwa kutoka gerezani.
Akifika mapema, nitakuja pamoja naye
kuwaona.
24 [b]Wasalimuni viongozi wenu wote na
watakatifu wote. Wale wa kutoka Italia
wanawasalimu.
25 [c]Neema iwe nanyi nyote. Amen.

[a]**13:23** 1The 3:2; Mdo 16:1; 1Tim 6:12
[b]**13:24** Ebr 13:7, 17; Mdo 18:2
[c]**13:25** Tit 3:15; Kol 4:18

# YAKOBO

1 [a]Yakobo, mtumwa wa Mungu na wa
Bwana Yesu Kristo:
Kwa makabila kumi na mawili
yaliyotawanyika ulimwenguni:
Salamu.

### *Imani Na Hekima*

2 [b]Ndugu zangu, hesabuni kuwa ni
furaha tupu mnapopatwa na majaribu
mbalimbali, 3 [c]kwa sababu mnajua ya kuwa
kujaribiwa kwa imani yenu huleta saburi.
4 [d]Saburi na iwe na kazi timilifu, ili mpate
kuwa wakamilifu, mmekamilishwa, bila
kupungukiwa na kitu chochote. 5 [e]Kama mtu
yeyote miongoni mwenu amepungukiwa
na hekima na amwombe Mungu, yeye
awapaye watu wote kwa ukarimu wala
hana kinyongo, naye atapewa. 6 [f]Lakini
anapoomba, lazima aamini wala asiwe na
shaka, kwa sababu mtu aliye na shaka ni
kama wimbi la bahari, lililochukuliwa na
upepo na kutupwa huku na huku. 7 Mtu
kama huyo asidhani ya kuwa atapata kitu
chochote kutoka kwa Bwana. 8 [g]Yeye ni
mtu mwenye nia mbili, mwenye kusitasita
katika njia zake zote.

### *Umaskini Na Utajiri*

9 [h]Ndugu asiye na cheo kikubwa yampasa
ajivunie hali hiyo maana ametukuzwa.
10 [i]Lakini yeye aliye tajiri afurahi kwa
kuwa ameshushwa, kwa sababu atatoweka
kama ua la shambani. 11 [j]Kwa maana
jua kali lenye kuchoma huchomoza na
kuliunguza, likayakausha majani, na ua lake
likapukutika, nao uzuri wake huharibika.
Vivyo hivyo tajiri naye atanyauka akiwa
anaendelea na shughuli zake.

### *Kujaribiwa*

12 [k]Heri mtu anayevumilia wakati wa
majaribu, kwa sababu akiisha kushinda
hilo jaribio atapewa taji la uzima Mungu
alilowaahidia wale wampendao.
13 Mtu anapojaribiwa asiseme,
"Ninajaribiwa na Mungu." Kwa maana
Mungu hawezi kujaribiwa na maovu wala
yeye hamjaribu mtu yeyote. 14 [l]Lakini kila
mtu hujaribiwa wakati anapovutwa na
kudanganywa na tamaa zake mwenyewe
zilizo mbaya. 15 [m]Basi ile tamaa mbaya
ikishachukua mimba, huzaa dhambi, nayo
ile dhambi ikikomaa, huzaa mauti.
16 [n]Ndugu zangu wapendwa,
msidanganyike. 17 [o]Kila kitolewacho kilicho
chema na kilicho kamili, hutoka juu, na
hushuka kutoka kwa Baba wa mianga,
ambaye kwake hakuna kubadilika, wala
kivuli cha kugeukageuka. 18 [p]Kwa mapenzi
yake mwenyewe alituzaa kwa neno la kweli,
kusudi tuwe kama mazao ya kwanza katika
viumbe vyake vyote.

### *Kusikia Na Kutenda*

19 [q]Ndugu zangu wapendwa, fahamuni
jambo hili: Kila mtu awe mwepesi wa
kusikiliza, lakini asiwe mwepesi wa kusema
wala wa kukasirika. 20 [r]Kwa maana hasira
ya mwanadamu haitendi haki ya Mungu.
21 [s]Kwa hiyo, ondoleeni mbali uchafu wote

---

[a]**1:1** Mdo 15:13; Rum 1:1; Tit 1:1; Mdo 26:7; Kum 32:26; Yn 7:35
[b]**1:2** Mt 5:12; Ebr 12:11; 10:34; Mdo 5:41; 1Pet 4:12, 16; 1:6
[c]**1:3** 1Pet 1:7; Ebr 10:36; Rum 5:3
[d]**1:4** 1Kor 2:6
[e]**1:5** 1Fal 3:9, 10; Mit 2:3-6; Dan 1:17; Mt 7:7; 1Fal 3:9, 10; Mit 2:3-6; Za 51:6; Dan 2:21; Mt 7:7
[f]**1:6** Mt 21:21; Mk 11:24; 1Tim 2:8
[g]**1:8** Za 119:113; Yak 4:8; 2Pet 2:14; 3:16
[h]**1:9** Mt 23:12
[i]**1:10** Ay 14:2; 1Kor 7:31
[j]**1:11** Za 102:4, 11; Isa 40:6-8
[k]**1:12** 1Kor 9:25; Kut 20:6; 1Kor 8:3
[l]**1:14** Mit 19:3; Rum 7:7-10
[m]**1:15** Mwa 3:6; Isa 59:4; Rum 6:23
[n]**1:16** 1Kor 6:9; Yak 2:5
[o]**1:17** Za 85:12; 102:27; Mt 3:6
[p]**1:18** Yn 1:13; Yer 2:3; Efe 1:12
[q]**1:19** Mit 10:19; Yak 1:16; 2:5; 3:3-12; Mhu 5:1, 2; Mit 14:17
[r]**1:20** Mt 5:22
[s]**1:21** Efe 4:22; 1:13; Kol 3:8; 1Pet 2:1; Mdo 13; 26; Rum 1:16; 1Kor 15:2

na uovu ambao umezidi kuwa mwingi,
mkalipokee kwa unyenyekevu lile Neno
lililopandwa ndani yenu ambalo laweza
kuokoa nafsi zenu.
22 [a]Basi kuweni watendaji wa Neno wala
msiwe wasikiaji tu, huku mkijidanganya
nafsi zenu. 23 [b]Kwa maana kama mtu ni
msikiaji tu wa Neno wala hatendi kile
linachosema, yeye ni kama mtu ajitazamaye
uso wake kwenye kioo 24 na baada ya kujiona
alivyo, huenda zake na mara husahau jinsi
alivyo. 25 Lakini yeye anayeangalia kwa
bidii katika sheria kamilifu, ile iletayo
uhuru, naye akaendelea kufanya hivyo
bila kusahau alichosikia, bali akalitenda,
atabarikiwa katika kile anachofanya.
26 [c]Kama mtu akidhani ya kuwa anayo
dini lakini hauzuii ulimi wake kwa hatamu,
hujidanganya moyoni mwake, wala dini
yake mtu huyo haifai kitu. 27 [d]Dini iliyo safi,
isiyo na uchafu, inayokubalika mbele za
Mungu Baba yetu, ndiyo hii: Kuwasaidia
yatima na wajane katika dhiki zao na
kujilinda usitiwe madoa na dunia.

*Onyo Kuhusu Upendeleo*

2 [e]Ndugu zangu, kama waaminio katika
imani ya Bwana wetu Yesu Kristo,
Bwana wa utukufu, msiwe na upendeleo
kwa watu. 2 [f]Kwa maana kama akija mtu
katika kusanyiko lenu akiwa amevaa pete
ya dhahabu na mavazi mazuri, pia akaingia
mtu maskini mwenye mavazi yaliyochakaa,
3 nanyi mkampa heshima yule aliyevaa
mavazi mazuri na kumwambia, "Keti
hapa mahali pazuri," lakini yule maskini
mkamwambia, "Wewe simama pale,"
au "Keti hapa sakafuni karibu na miguu
yangu," 4 [g]je, hamjawabagua na kuwa
mahakimu mioyoni mwenu mkihukumu
kwa mawazo yenu maovu?
5 [h]Ndugu zangu, sikilizeni: Je, Mungu
hakuwachagua wale walio maskini machoni
pa ulimwengu kuwa matajiri katika imani
na kuurithi Ufalme aliowaahidi wale
wampendao? 6 [i]Lakini ninyi mmemdharau
yule aliye maskini. Je, hao matajiri si
ndio wanaowadhulumu na kuwaburuta
mahakamani? 7 Je, si wao wanaolikufuru
Jina lile lililo bora sana mliloitiwa?
8 [j]Kama kweli mnaitimiza ile sheria ya
kifalme inayopatikana katika Maandiko
isemayo, "Mpende jirani yako kama
unavyoipenda nafsi yako," mnafanya
vyema. 9 [k]Lakini kama mnakuwa na
upendeleo kwa watu, mnatenda dhambi,
na sheria inawahukumu kuwa ninyi ni
wakosaji. 10 [l]Kwa maana mtu yeyote
anayeishika sheria yote lakini akajikwaa
katika kipengele kimoja tu, ana hatia ya
kuivunja sheria yote. 11 [m]Kwa sababu yeye
aliyesema, "Usizini," alisema pia, "Usiue."
Basi kama huzini lakini unaua, umekuwa
mvunjaji wa sheria.
12 [n]Hivyo semeni na kutenda kama watu
watakaohukumiwa kwa sheria ile iletayo
uhuru. 13 [o]Kwa kuwa hukumu bila huruma
itatolewa kwa mtu yeyote asiyekuwa na
huruma. Huruma huishinda hukumu.

*Imani Na Matendo*

14 [p]Ndugu zangu, yafaa nini ikiwa mtu
atadai kuwa anayo imani lakini hana
matendo? Je, imani kama hiyo yaweza
kumwokoa? 15 [q]Ikiwa ndugu yako au dada
hana mavazi wala chakula, 16 [r]mmoja wenu
akamwambia, "Enenda zako kwa amani,
ukaote moto na kushiba," pasipo kumpatia
yale mahitaji ya mwili aliyopungukiwa,

[a]**1:22** Mt 7:21; Yak 2:14-20
[b]**1:23** Lk 6:47; Mdo 2:14
[c]**1:26** Za 39:1; 1Pet 3:10
[d]**1:27** Mt 25:36; Za 146:9; Isa 1:17, 23; Rum 12:2; 2Pet 2:20
[e]**2:1** Mdo 7:2; 1Kor 2:8; Mit 24:23; Mdo 10:34
[f]**2:2** Ebr 10:25
[g]**2:4** Yn 7:24
[h]**2:5** Yak 1:16, 19; Ay 34:19; 1Kor 1:26-28; Lk 12:21; Ufu 2:9; Yos 1:12
[i]**2:6** 1Kor 11:22; Mdo 8:3; 16:19
[j]**2:8** Law 19:18; Mt 5:43
[k]**2:9** Kum 1:17; Yak 2:1
[l]**2:10** Mt 5:19; Gal 5:3
[m]**2:11** Kut 20:14; Kum 5:18; 5:17; Kut 20:13
[n]**2:12** Yak 1:25; Mt 16:27
[o]**2:13** Mt 9:13; Lk 6:37
[p]**2:14** Mt 7:26; Yak 1:22-25
[q]**2:15** Mt 25:35, 36; Ay 31:19; Lk 3:11
[r]**2:16** Lk 3:11; 1Yn 3:17, 18

yafaa nini? 17 [a]Vivyo hivyo, imani peke yake
kama haikuambatana na matendo, imekufa.
18 [b]Lakini mtu mwingine atasema, “Wewe
unayo imani; mimi ninayo matendo.”

Nionyeshe imani yako pasipo matendo
nami nitakuonyesha imani yangu kwa
matendo. 19 [c]Unaamini kwamba kuna
Mungu mmoja. Vyema! Hata mashetani
yanaamini hivyo na kutetemeka.
20 [d]Ewe mpumbavu! Je, wataka kujua
kwamba imani bila matendo haifai kitu?
21 [e]Je, Abrahamu baba yetu hakuhesabiwa
haki kwa kile alichotenda, alipomtoa
mwanawe Isaki madhabahuni? 22 [f]Unaona
jinsi ambavyo imani yake na matendo
yake vilikuwa vinatenda kazi pamoja,
nayo imani yake ikakamilishwa na kile
alichotenda. 23 [g]Kwa njia hiyo yakatimizwa
yale Maandiko yasemayo, “Abrahamu
alimwamini Mungu na ikahesabiwa kwake
kuwa haki,” naye akaitwa rafiki wa Mungu.
24 Mnaona ya kwamba mtu huhesabiwa haki
kwa yale anayotenda wala si kwa imani
peke yake.
25 [h]Vivyo hivyo, hata Rahabu, yule
kahaba, hakuhesabiwa haki kwa yale
aliyotenda alipowapokea wale wapelelezi
na kuwaambia waende njia nyingine?
26 Kama vile ambavyo mwili pasipo roho
umekufa, kadhalika nayo imani pasipo
matendo imekufa.

### *Kuufuga Ulimi*

3 [i]Ndugu zangu, msiwe walimu wengi,
kwa maana mnafahamu kwamba sisi
tufundishao tutahukumiwa vikali zaidi.
2 [j]Sisi sote tunajikwaa katika mambo mengi.
Ikiwa mtu yeyote hakosei kamwe katika
yale anayosema, yeye ni mkamilifu, naye
anaweza kuuzuia pia na mwili wake wote.
3 [k]Tunapotia lijamu kwenye vinywa vya
farasi ili kuwafanya watutii, tunaweza
kuigeuza miili yao yote. 4 Au angalia
pia meli, ingawa ni kubwa sana, nazo
huchukuliwa na upepo mkali, lakini
hugeuzwa kwa usukani mdogo sana,
kokote anakotaka nahodha. 5 [l]Vivyo hivyo
ulimi ni kiungo kidogo sana katika mwili,
lakini hujivuna majivuno makuu. Fikirini
jinsi moto mdogo unavyoweza kuteketeza
msitu mkubwa! 6 [m]Ulimi pia ni moto, ndio
ulimwengu wa uovu kati ya viungo vya
mwili. Ulimi huutia mwili wote wa mtu
unajisi na kuuwasha moto mfumo mzima
wa maisha yake, nao wenyewe huchomwa
moto wa jehanamu.
7 Kwa maana kila aina ya wanyama,
ndege, wanyama watambaao na viumbe
vya baharini vinafugika na vimefugwa na
binadamu, 8 [n]lakini hakuna mtu awezaye
kuufuga ulimi. Ni uovu usiotulia, umejaa
sumu iletayo mauti.
9 [o]Kwa ulimi tunamhimidi Bwana, yaani
Baba yetu, na kwa huo twawalaani watu
walioumbwa kwa mfano wa Mungu.
10 Katika kinywa kile kile hutoka baraka
na laana. Ndugu zangu, haistahili kuwa
hivyo. 11 [p]Je, chemchemi yaweza kutoa
katika tundu moja maji matamu na maji
ya chumvi? 12 [q]Je, ndugu zangu, mtini
waweza kuzaa zeituni, au mzabibu kuzaa
tini? Wala chemchemi ya maji ya chumvi
haiwezi kutoa maji matamu.

### *Aina Mbili Za Hekima*

13 [r]Ni nani aliye na hekima na ufahamu
miongoni mwenu? Basi na aonyeshe hiyo
kwa maisha yake mema na kwa matendo
yake yaliyotendwa kwa unyenyekevu

---

[a]**2:17** Yak 2:20, 26; Gal 5:6
[b]**2:18** Rum 3:28; Mt 7:16, 17; Yak 3:13
[c]**2:19** Kum 6:4; Mt 12:29; 8:29; Lk 4:34
[d]**2:20** Yak 2:17, 26
[e]**2:21** Mwa 22:9, 12
[f]**2:22** Ebr 11:17; 1The 1:3
[g]**2:23** Mwa 15:6; Rum 4:3; 2Nya 20:7; Isa 41:8
[h]**2:25** Ebr 11:31
[i]**3:1** 1Fal 8:46; 1Yn 1:8; Mit 10:19; 1Pet 3:10; Mt 12:37; Yak 1:26
[j]**3:2** Za 12:3, 4; 73:8, 9
[k]**3:3** Za 32:9
[l]**3:5** Mt 15:11, 18, 19; Za 12:3, 4; 73:8, 9
[m]**3:6** Mit 16:27; Mt 15:11, 18, 19; 5:22
[n]**3:8** Za 140:10; Rum 3:13
[o]**3:9** Mwa 1:26-27
[p]**3:11** Kut 20:14; Kum 5:8; 5:17; Kut 5:18
[q]**3:12** Yak 1:25
[r]**3:13** Mt 9:13; Lk 6:37

utokanao na hekima. 14 [a]Lakini ikiwa mna
wivu na ni wenye chuki na ugomvi mioyoni
mwenu, msijisifu kwa ajili ya hayo wala
msiikatae kweli. 15 [b]Hekima ya namna
hiyo haishuki kutoka mbinguni, bali ni ya
kidunia, isiyo ya kiroho, na ya kishetani.
16 [c]Kwa maana panapokuwa na wivu na
ubinafsi, ndipo penye machafuko na uovu
wa kila namna.
17 Lakini hekima itokayo mbinguni
kwanza ni safi, kisha inapenda amani, tena
ni ya upole, iliyo tayari kusikiliza wengine
kwa unyenyekevu, iliyojaa huruma na
matunda mema, isiyopendelea mtu, tena
isiyokuwa na unafiki. 18 [d]Mavuno ya haki
hupandwa katika amani na wale wafanyao
amani.

*Jinyenyekezeni Kwa Mungu*

4 [e]Ni kitu gani kinachosababisha mapigano
na ugomvi miongoni mwenu? Je, haya
hayatokani na tamaa zenu zinazoshindana
ndani yenu? 2 [f]Mnatamani lakini hampati,
kwa hiyo mwaua. Mwatamani kupata
lakini hampati vile mnavyotaka, kwa hiyo
mnajitia katika magomvi na mapigano.
Mmepungukiwa kwa sababu hammwombi
Mungu. 3 [g]Mnapoomba hampati kwa sababu
mnaomba kwa nia mbaya, ili mpate
kuvitumia hivyo mtakavyopata kwa tamaa
zenu.
4 [h]Ninyi wanaume na wanawake wazinzi,
hamjui ya kwamba urafiki na dunia ni uadui
na Mungu? Kwa hiyo mtu yeyote anayetaka
kuwa rafiki wa dunia hufanyika adui wa
Mungu. 5 [i]Au mwadhani kwamba Andiko
lasema bure kuwa huyo Roho ambaye
Mungu amemweka ndani yetu hututamani
kiasi cha kuona wivu? 6 [j]Lakini yeye
hutupatia neema zaidi. Hii ndiyo sababu
Andiko husema:

“Mungu huwapinga wenye kiburi,
lakini huwapa wanyenyekevu
neema.”

7 [k]Basi mtiini Mungu. Mpingeni ibilisi,
naye atawakimbia. 8 [l]Mkaribieni Mungu,
naye atawakaribia ninyi. Itakaseni
mikono yenu ninyi wenye dhambi, na
kuisafisha mioyo yenu ninyi wenye nia
mbili. 9 [m]Huzunikeni, ombolezeni na
kulia. Kicheko chenu na kigeuzwe kuwa
kuomboleza, na furaha yenu kuwa huzuni.
10 [n]Jinyenyekezeni mbele za Bwana, naye
atawainua.

*Onyo Kuhusu Kuhukumu Wengine*

11 [o]Ndugu, msineneane mabaya ninyi
kwa ninyi. Mtu yeyote anayesema mabaya
dhidi ya ndugu yake au kumhukumu
anasema dhidi ya sheria na kuihukumu.
Unapoihukumu sheria, basi huishiki sheria
bali umekuwa hakimu wa kuihukumu
hiyo sheria. 12 [p]Yuko Mtoa sheria mmoja
tu na yeye peke yake ndiye Hakimu, ndiye
awezaye kuokoa au kuangamiza. Lakini
wewe ni nani hata umhukumu jirani yako?

*Kujivuna Kwa Ajili Ya Kesho*

13 [q]Basi sikilizeni ninyi msemao, “Leo
au kesho tutakwenda katika mji huu ama
ule tukae humo mwaka mmoja, tufanye
biashara na kupata faida.” 14 [r]Lakini hamjui
hata litakalotukia kesho. Maisha yenu ni
nini? Ninyi ni ukungu ambao huonekana
kwa kitambo kidogo kisha hutoweka.
15 [s]Badala yake, inawapasa kusema, “Kama
Bwana akipenda, tutaishi na kufanya hili
ama lile.” 16 [t]Kama ilivyo sasa, mnajisifu

[a]**3:14** Mt 6:27; Yak 1:22-25
[b]**3:15** Mt 25:35, 36
[c]**3:16** Lk 3:11; 1Yn 3:17, 18
[d]**3:18** Rum 3:28; Mt 7:16, 18
[e]**4:1** Tit 3:9; Rum 7:23
[f]**4:2** Mt 5:21, 22; Yak 5:6; 1Yn 3:15
[g]**4:3** Mt 7:7; Za 66:18; 1Yn 5:14
[h]**4:4** Yak 1:27; Rum 8:7; Yn 15:19
[i]**4:5** 1Kor 6:19; Mwa 6:5; 8:21; Hes 11:29; Mit 21:10
[j]**4:6** Za 138:6; Mt 23:12
[k]**4:7** Efe 6:11; 1Pet 5:6-9
[l]**4:8** Ebr 7:19; Isa 1:16; Za 119:113
[m]**4:9** Lk 6:25; Mt 5:4
[n]**4:10** Ay 22:29; Mt 23:12; Lk 14:11; 1Pet 5:6
[o]**4:11** Rum 1:30; 2Kor 12:20; Mt 7:1; Yak 1:22
[p]**4:12** Mt 10:28; 7:1
[q]**4:13** Lk 12:18-20
[r]**4:14** Za 39:5; Isa 2:22
[s]**4:15** Mdo 18:21
[t]**4:16** 1Kor 5:6

na kujigamba. Kujisifu kwa namna hiyo ni
uovu. 17 [a]Basi mtu yeyote anayejua jema
limpasalo kutenda, lakini asilitende, mtu
huyo anatenda dhambi.

### *Onyo Kwa Matajiri*

5 [b]Basi sikilizeni, ninyi matajiri, lieni na
kuomboleza kwa ajili ya hali mbaya
sana inayowajia. 2 [c]Utajiri wenu umeoza na
mavazi yenu yameliwa na nondo. 3 Dhahabu
yenu na fedha yenu vimeliwa na kutu. Kutu
yake itashuhudia dhidi yenu nayo itaila miili
yenu kama vile moto. Mmejiwekea hazina
kwa ajili ya siku za mwisho. 4 [d]Angalieni!
Ule ujira wa vibarua waliolima mashamba
yenu mliouzuia kwa hila unapiga kelele
dhidi yenu na vilio vya wavunaji vimefika
masikioni mwa Bwana Mwenye Nguvu
Zote. 5 [e]Mmeishi duniani kwa anasa na kwa
starehe, mmejinenepesha tayari kwa siku
ya kuchinjwa. 6 [f]Mmewahukumu na kuwaua
watu wenye haki, waliokuwa hawapingani
nanyi.

### *Uvumilivu Katika Mateso*

7 [g]Kwa hiyo, ndugu zangu, vumilieni
hadi kuja kwake Bwana. Angalieni jinsi
mkulima angojavyo ardhi itoe mavuno yake
yaliyo ya thamani na jinsi anavyovumilia
kwa ajili ya kupata mvua za kwanza na
za mwisho. 8 [h]Ninyi nanyi vumilieni, tena
simameni imara, kwa sababu kuja kwa
Bwana kumekaribia. 9 [i]Ndugu zangu,
msinung'unikiane msije mkahukumiwa.
Hakimu amesimama mlangoni!
10 [j]Ndugu zangu, waangalieni manabii
walionena kwa Jina la Bwana, ili kuwa
mfano wa uvumilivu katika kukabiliana na
mateso. 11 [k]Kama mnavyojua, tunawahesabu
kuwa wabarikiwa wale waliovumilia.
Mmesikia habari za uvumilivu wake Ayubu
na mmeona kile ambacho hatimaye Bwana
alimtendea. Bwana ni mwingi wa huruma,
na amejaa rehema.
12 [l]Zaidi ya yote, ndugu zangu, msiape,
iwe kwa mbingu au kwa dunia, au kwa
kitu kingine chochote. "Ndiyo" yenu na iwe
ndiyo, na "Hapana" yenu iwe hapana, la
sivyo mtahukumiwa.

### *Maombi Ya Imani*

13 [m]Je, mtu yeyote miongoni mwenu
amepatwa na taabu? Basi inampasa aombe.
Je, kuna yeyote mwenye furaha? Basi
na aimbe nyimbo za kusifu. 14 [n]Je, kuna
yeyote miongoni mwenu aliye mgonjwa?
Basi inampasa awaite wazee wa kanisa
wamwombee na kumpaka mafuta kwa
Jina la Bwana. 15 [o]Kule kuomba kwa imani
kutamwokoa huyo mgonjwa, naye Bwana
atamwinua na kama ametenda dhambi,
atasamehewa. 16 [p]Kwa hiyo ungamianeni
dhambi zenu ninyi kwa ninyi na kuombeana
ili mpate kuponywa. Maombi ya mwenye
haki yana nguvu tena yanafaa sana.
17 [q]Eliya alikuwa mwanadamu kama
sisi. Akaomba kwa bidii kwamba mvua
isinyeshe, nayo haikunyesha juu ya nchi
kwa muda wa miaka mitatu na miezi
sita. 18 [r]Kisha akaomba tena, nazo mbingu
zikatoa mvua nayo ardhi ikatoa mazao
yake.
19 [s]Ndugu zangu, yeyote miongoni mwenu
akipotoka na kuicha kweli, naye akarejezwa
na mtu mwingine, 20 [t]hamna budi kujua
kwamba yeyote amrejezaye mwenye

[a] **4:17** Lk 12:47; Yn 9:41
[b] **5:1** 1Tim 6:9; Mit 11:28; Lk 6:24
[c] **5:2** Za 39:11; Ay 13:22; Mt 6:20; Yak 2:2
[d] **5:4** Mt 3:5; Kum 24:15; Rum 9:29
[e] **5:5** Yer 12:3; 25:34
[f] **5:6** Mit 3:34; Yak 2:6; Ebr 10:38; Yak 4:2
[g] **5:7** Yer 5:24; Yoe 2:23
[h] **5:8** Rum 13:11; 1Pet 4:7
[i] **5:9** Yak 4:11; Za 94:2; 1Kor 4:5; Mt 24:33
[j] **5:10** Mt 5:12; Ebr 11:25
[k] **5:11** Mt 5:10; Ay 2:10; Ebr 10:36; Ay 42:10; 12:17; Kut 34:6
[l] **5:12** Mt 5:31-34; Yak 1:25
[m] **5:13** Za 50:15; Kol 3:16
[n] **5:14** Za 23:5; Mdo 11:30; Isa 1:6; Mk 6:13; 16:18; Lk 10:38
[o] **5:15** Yak 1:6; Isa 33:24; Mt 9:2
[p] **5:16** Mdo 19:18; Ebr 12:13; Mt 7:7
[q] **5:17** Mdo 14:15; 1Fal 17:1; Lk 4:25
[r] **5:18** 1Fal 18:41-45
[s] **5:19** Yak 3:14; Mt 18:15
[t] **5:20** Rum 11:14; 1Pet 4:8

dhambi kutoka upotovu wake, ataiokoa
roho ya huyo mwenye dhambi kutoka mauti
na kusitiri wingi wa dhambi.

# 1 PETRO

*Salamu*

1 [a]Petro, mtume wa Yesu Kristo:
Kwa wateule wa Mungu, wageni
katika ulimwengu, waliotawanyika kote
katika Ponto, Galatia, Kapadokia, Asia na
Bithinia. 2 [b]Ni ninyi ambao mlichaguliwa
tangu mwanzo na Mungu Baba kulingana
na alivyotangulia kuwajua, kupitia kwa kazi
ya utakaso wa Roho, katika utiifu kwa Yesu
Kristo na kunyunyiziwa damu yake:
Neema na amani ziwe kwenu kwa wingi.

*Tumaini Lenye Uzima*

3 [c]Ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana
wetu Yesu Kristo! Kwa rehema zake kuu
ametuzaa sisi mara ya pili katika tumaini
lenye uzima kupitia kwa kufufuka kwa
Yesu Kristo kutoka kwa wafu, 4 [d]ili tuupate
urithi usioharibika, usio na uchafu, ule
usionyauka: uliotunzwa mbinguni kwa
ajili yenu, 5 [e]ninyi ambao mnalindwa na
nguvu za Mungu kwa njia ya imani, hadi
uje ule wokovu ulio tayari kufunuliwa
nyakati za mwisho. 6 [f]Katika hili mnafurahi
sana, ingawa sasa kwa kitambo kidogo
mmehuzunishwa kwa majaribu ya namna
nyingi. 7 [g]Haya yamewajia ili kwamba imani
yenu, iliyo ya thamani kuliko dhahabu
ipoteayo, ingawa hujaribiwa kwa moto,
ionekane kuwa halisi na imalizie katika
sifa, utukufu na heshima wakati Yesu Kristo
atadhihirishwa. 8 [h]Ingawa hamjamwona,
mnampenda; tena ingawa sasa hammwoni,
mnamwamini na kujawa na furaha
isiyoneneka yenye utukufu usioelezeka.
9 [i]Maana mnaupokea wokovu wa roho zenu,
ambao ndio lengo la imani yenu.
10 [j]Kwa habari ya wokovu huu, wale
manabii waliosema kuhusu neema ambayo
ingewajia ninyi, walitafuta kwa bidii na
kwa uangalifu mkubwa, 11 [k]wakijaribu kujua
ni wakati upi na katika mazingira gani
ambayo Roho wa Kristo aliyekuwa ndani
yao alionyesha, alipotabiri kuhusu mateso
ya Kristo na utukufu ule ambao ungefuata.
12 [l]Walidhihirishiwa kwamba walikuwa
hawajihudumii wao wenyewe, bali
waliwahudumia ninyi, waliponena kuhusu
mambo hayo, ambayo sasa yamehubiriwa
kwenu na wale waliowahubiria ninyi Injili
kwa Roho Mtakatifu aliyetumwa kutoka
mbinguni. Hata malaika wanatamani
kuyafahamu mambo haya.

*Mwito Wa Kuishi Maisha Matakatifu*

13 [m]Kwa hiyo, tayarisheni nia zenu
kwa kazi; mwe na kiasi, mkitumainia
kikamilifu ile neema mtakayopewa Yesu
Kristo atakapodhihirishwa. 14 [n]Kama watoto
watiifu, msifuate tamaa zenu mbaya wakati
mlipoishi kwa ujinga. 15 [o]Bali kama yeye
aliyewaita alivyo mtakatifu, nanyi kuweni
watakatifu katika mwenendo wenu wote.
16 [p]Kwa maana imeandikwa: "Kuweni
watakatifu, kwa kuwa mimi ni mtakatifu."
17 [q]Kwa sababu mnamwita Baba
ahukumuye kila mtu kulingana na matendo
yake pasipo upendeleo, enendeni kwa
hofu ya kumcha Mungu wakati wenu wa
kukaa hapa duniani kama wageni. 18 [r]Kwa

---

[a]**1:1** 2Pet 1:1; Mt 24:22; Mdo 16:7
[b]**1:2** Rum 8:29; 2The 2:13; Ebr 10:22; 12:24
[c]**1:3** 1Kor 1:3; Efe 1:3; Tit 3:5; Yak 1:18; 1Pet 3:21
[d]**1:4** 1Tim 4:8; Mdo 20:32; Rum 8:17; 1Pet 5:4; Kol 1:5
[e]**1:5** 1Sam 2:9; Yn 10:28; Rum 11:14; 8:18
[f]**1:6** Rum 5:2; 1Pet 5:10; 4:12
[g]**1:7** Mit 17:3; Isa 48:10; 1The 2:19
[h]**1:8** Yn 20:29; 1Yn 4:10; 2Kor 5:7; Ebr 11:1, 27
[i]**1:9** Rum 6:22
[j]**1:10** Mt 22:24; 3:17
[k]**1:11** Mdo 16:7; Za 22:1; Isa 52:13; 53:12; Lk 24:26
[l]**1:12** Efe 3:10; Lk 2:13
[m]**1:13** Mdo 24:25; 1Pet 1:3, 21; Ebr 3:6; 1Pet 1:7, 10; 1Kor 1:7; Efe 5:19; Kol 3:16
[n]**1:14** Rum 12:2; Efe 4:18
[o]**1:15** Isa 35:8; 1The 4:7; 1Yn 3:3
[p]**1:16** Law 19:2; 20:7
[q]**1:17** Mdo 10:34; Ebr 12:28
[r]**1:18** Mt 20:28; 1Kor 6:20

maana mnafahamu kwamba mlikombolewa
kutoka mwenendo wenu usiofaa ambao
mliurithi kutoka kwa baba zenu, si kwa
vitu viharibikavyo kama fedha na dhahabu,
[19] [a]bali kwa damu ya thamani ya Kristo,
yule Mwana-Kondoo asiye na dosari
wala doa. [20] [b]Yeye alichaguliwa kabla ya
kuwekwa kwa misingi ya ulimwengu,
lakini akadhihirishwa katika siku hizi za
mwisho kwa ajili yenu. [21] [c]Kupitia kwake
mmemwamini Mungu, aliyemfufua kutoka
kwa wafu na akampa utukufu, ili imani
yenu na tumaini lenu ziwe kwa Mungu.

[22] [d]Basi kwa kuwa mmejitakasa nafsi zenu
kwa kuitii ile kweli hata mkawa na upendo
wa ndugu usio na unafiki, basi pendaneni
kwa dhati kutoka moyoni. [23] [e]Kwa maana
mmezaliwa upya, si kwa mbegu ile
iharibikayo, bali kwa ile isiyoharibika,
kupitia kwa neno la Mungu lililo hai na
linalodumu milele. [24] [f]Maana,

“Wanadamu wote ni kama majani,
nao utukufu wao ni kama maua ya
kondeni;
majani hunyauka na maua
huanguka,
[25] [g]lakini neno la Bwana ladumu
milele.”

Hili ndilo neno lililohubiriwa kwenu.

### *Jiwe Lililo Hai Na Watu Waliochaguliwa*

2 [h]Kwa hiyo, wekeni mbali nanyi uovu wote
na udanganyifu wote, unafiki, wivu na
masingizio ya kila namna. [2] [i]Kama watoto
wachanga, waliozaliwa sasa, yatamanini
maziwa ya kiroho yasiyochanganywa na
kitu kingine chochote, ili kwa hayo mpate
kukua katika wokovu, [3] [j]ikiwa kweli
mmeonja ya kwamba Bwana ni mwema.

[4] [k]Mnapokuja kwake, yeye aliye Jiwe
lililo hai, lililokataliwa na wanadamu bali
kwa Mungu ni teule na la thamani kwake,
[5] [l]ninyi nanyi, kama mawe yaliyo hai,
mnajengwa kuwa nyumba ya kiroho, ili
mpate kuwa ukuhani mtakatifu, mkitoa
dhabihu za kiroho zinazokubaliwa na
Mungu kwa njia ya Yesu Kristo. [6] [m]Kwa
maana imeandikwa katika Maandiko:

“Tazama, naweka katika Sayuni,
jiwe la pembeni teule lenye
thamani,
na yeyote atakayemwamini
hataaibika kamwe.”

[7] [n]Kwenu ninyi mnaoamini, jiwe hili ni la
thamani. Lakini kwao wasioamini,

“Jiwe walilolikataa waashi
limekuwa jiwe kuu la pembeni,”

[8] [o]tena,

“Jiwe lenye kuwafanya watu
wajikwae,
na mwamba wa kuwaangusha.”

Wanajikwaa kwa sababu hawakulitii lile
neno, kama walivyowekewa tangu zamani.

[9] [p]Lakini ninyi ni taifa teule, ukuhani wa
kifalme, taifa takatifu, watu walio milki ya
Mungu, mlioitwa ili kutangaza sifa zake
yeye aliyewaita kutoka gizani mkaingie
katika nuru yake ya ajabu. [10] [q]Mwanzo ninyi
mlikuwa si taifa, lakini sasa ninyi ni taifa
la Mungu. Mwanzo mlikuwa hamjapata
rehema, lakini sasa mmepata rehema.

[11] [r]Wapenzi, ninawasihi, mkiwa kama
wageni na wapitaji hapa ulimwenguni,
epukeni tamaa mbaya za mwili ambazo
hupigana vita na roho zenu. [12] [s]Kuweni na
mwenendo mzuri mbele ya watu wasiomjua
Mungu, ili kama wanawasingizia kuwa

[a]**1:19** Yn 1:29; Kut 12:5
[b]**1:20** Mt 25:34; Ebr 9:26
[c]**1:21** Rum 10:9
[d]**1:22** Yak 4:8; Rum 12:10; Ebr 13:1
[e]**1:23** Yn 1:13; Ebr 4:12
[f]**1:24** Za 103:15; Isa 40:6
[g]**1:25** Isa 40:6-8; Yak 1:10-11
[h]**2:1** Efe 4:22; Yak 4:11
[i]**2:2** 1Kor 3:2; Ebr 5:12-13; Efe 4:15-16
[j]**2:3** Za 34:8; Ebr 6:5
[k]**2:4** Za 118:22; Mt 21:42; Mdo 4:11
[l]**2:5** Mit 9:1; Efe 2:20-22; 1Tim 3:15; Kut 19:6; Ufu 5:10; Ebr 13:15
[m]**2:6** Efe 2:20; Rum 10:11
[n]**2:7** 2Kor 2:16; Mdo 4:11
[o]**2:8** Isa 8:14; 1Kor 1:23; Rum 9:22
[p]**2:9** 1Sam 12:22; Kut 19:6; Mdo 26:18
[q]**2:10** Rum 9:25-26; Hos 1:9, 10; 2:23
[r]**2:11** Rum 13:14; Yak 4:1
[s]**2:12** Tit 2:8, 14; Mt 5:16; 9:8

watenda mabaya, wayaone matendo yenu mema nao wamtukuze Mungu siku atakapokuja kwetu.

*Kuwatii Wenye Mamlaka*

13 [a]Kwa ajili ya Bwana, tiini kila mamlaka iliyowekwa na wanadamu: Kwa mfalme kwani ndiye aliye na mamlaka ya juu zaidi, 14 [b]au kwa maafisa aliowaweka, kwa kuwa mfalme amewatuma ili kuwaadhibu wale wanaokosa, na kuwapongeza wale watendao mema. 15 [c]Kwa maana ni mapenzi ya Mungu kwamba kwa kutenda mema mnyamazishe maneno ya kijinga ya watu wapumbavu. 16 [d]Ishini kama watu huru, lakini msitumie uhuru wenu kama kisingizio cha kutenda uovu, bali ishini kama watumishi wa Mungu. 17 [e]Mheshimuni kila mtu ipasavyo: Wapendeni jamaa ya ndugu waumini, mcheni Mungu, mpeni heshima mfalme.

18 [f]Ninyi watumwa, watiini mabwana zenu kwa heshima yote, si wale mabwana walio wema na wapole peke yao, bali pia wale walio wakali. 19 [g]Kwa maana ni jambo la sifa kama mtu akivumilia anapoteswa kwa uonevu kwa ajili ya Mungu. 20 [h]Kwani ni faida gani kwa mtu kustahimili anapopigwa kwa sababu ya makosa yake? Lakini kama mkiteswa kwa sababu ya kutenda mema, nanyi mkastahimili, hili ni jambo la kusifiwa mbele za Mungu.

*Mfano Wa Mateso Ya Kristo*

21 [i]Ninyi mliitwa kwa ajili ya haya, kwa sababu Kristo naye aliteswa kwa ajili yenu, akiwaachia kielelezo, ili mzifuate nyayo zake.

22 [j]"Yeye hakutenda dhambi,
wala hila haikuonekana kinywani
mwake."

23 [k]Yeye alipotukanwa, hakurudisha matukano; alipoteswa, hakutishia, bali alijikabidhi kwa yeye ahukumuye kwa haki. 24 [l]Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti, ili tufe kwa mambo ya dhambi, bali tupate kuishi katika haki. Kwa kupigwa kwake, ninyi mmeponywa. 25 [m]Kwa maana mlikuwa mmepotea kama kondoo, lakini sasa mmerudi kwa Mchungaji na Mwangalizi wa roho zenu.

*Mafundisho Kwa Wake Na Waume*

3 [n]Kadhalika enyi wake, watiini waume zenu, ili kama kunao wasioamini lile neno, wapate kuvutwa na mwenendo wa wake zao pasipo neno, 2 [o]kwa kuuona utakatifu na uchaji wa Mungu katika maisha yenu. 3 [p]Kujipamba kwenu kusiwe kwa nje tu, kama vile kusuka nywele, kuvalia vitu vilivyofanyizwa kwa dhahabu na kwa mavazi. 4 [q]Badala yake, kujipamba kwenu kuwe katika utu wenu wa moyoni, yaani uzuri usioharibika wa roho ya upole na utulivu, ambayo ni ya thamani sana machoni pa Mungu. 5 [r]Kwa kuwa hivi ndivyo walivyokuwa wakijipamba wanawake watakatifu wa zamani, waliomtumaini Mungu. Wao walikuwa ni watiifu kwa waume zao, 6 [s]kama Sara alivyomtii mumewe Abrahamu, hata akamwita bwana. Ninyi ni watoto wa Sara kama mkitenda yaliyo mema, bila kuogopa jambo lolote.

---

[a]**2:13** Tit 3:1; Rum 13:1; Mt 22:21
[b]**2:14** Rum 13:3-4
[c]**2:15** 1Pet 3:17; 4:19
[d]**2:16** Yn 8:32; Rum 6:22
[e]**2:17** Rum 12:10; Mit 24:21; 1Pet 2:18; Efe 6:5; Yak 3:17
[f]**2:18** 1Kor 6:20; 7:23; Eze 20:18; 1Pet 4:3
[g]**2:19** 1Pet 3:14-17; Mt 5:10; Rum 13:5; 1Pet 3:14
[h]**2:20** 1Pet 3:14; 4:14, 15
[i]**2:21** Flp 1:29; Mt 11:29
[j]**2:22** Isa 53:7-9
[k]**2:23** Lk 23:46
[l]**2:24** Isa 53:4-11; Rum 6:2; Za 103:3; Ebr 12:13
[m]**2:25** Isa 53:6; Yn 10:11
[n]**3:1** 1Pet 2:18; Efe 5:22; 1Kor 7:16
[o]**3:2** 1Pet 2:12
[p]**3:3** Isa 3:18-23; 1Tim 2:9; 1Pet 3:4; Rum 7:22; Efe 3:16
[q]**3:4** Za 45:13; Rum 2:29; 7:22; 2Kor 4:16
[r]**3:5** 1Tim 5:5
[s]**3:6** Mwa 18:12

7 [a]Vivyo hivyo ninyi waume, kaeni na
wake zenu kwa akili, nanyi wapeni heshima
mkitambua ya kuwa wao ni wenzi walio
dhaifu, na kama warithi pamoja nanyi wa
kipawa cha neema cha uzima, ili kusiwepo
na chochote cha kuzuia maombi yenu.

### *Kuteseka Kwa Kutenda Mema*

8 [b]Hatimaye, ninyi nyote kuweni na nia
moja, wenye kuhurumiana, mkipendana
kama ndugu, na mwe wasikitivu na
wanyenyekevu. 9 [c]Msilipe ovu kwa ovu, au
jeuri kwa jeuri, bali barikini, kwa maana
hili ndilo mliloitiwa ili mpate kurithi
baraka. 10 [d]Kwa maana,

“Yeyote apendaye uzima
na kuona siku njema,
basi auzuie ulimi wake usinene
mabaya,
na midomo yake isiseme hila.
11 [e]Mtu huyo lazima aache uovu,
akatende mema;
lazima aitafute amani na
kuifuatilia sana.
12 [f]Kwa maana macho ya Bwana
huwaelekea wenye haki,
na masikio yake yako makini
kusikiliza maombi yao.
Bali uso wa Bwana uko kinyume
na watendao maovu.”

### *Kuvumilia Mateso*

13 [g]Basi, ni nani atakayewadhuru
mkiwa wenye juhudi katika kutenda
mema? 14 [h]Lakini mmebarikiwa hata kama
ikiwalazimu kuteseka kwa ajili ya haki.
“Msiogope vitisho vyao, wala msiwe na
wasiwasi.” 15 [i]Bali mtakaseni Kristo kuwa
Bwana mioyoni mwenu. Siku zote mwe
tayari kumjibu mtu yeyote atakayewauliza
kuhusu sababu ya tumaini lililomo ndani
yenu. Lakini fanyeni hivyo kwa upole na
kwa heshima, 16 [j]mkizitunza dhamiri zenu
ziwe safi, ili wale wasemao mabaya dhidi
ya mwenendo wenu mzuri katika Kristo
waaibike kwa ajili ya masingizio yao.

17 [k]Kwa maana ni afadhali kupata mateso
kwa ajili ya kutenda mema, kama kuteseka
huko ndiyo mapenzi ya Mungu, kuliko
kuteseka kwa kutenda maovu. 18 [l]Kwa kuwa
Kristo naye aliteswa mara moja tu kwa ajili
ya dhambi, mwenye haki kwa ajili ya wasio
haki, ili awalete ninyi kwa Mungu. Mwili
wake ukauawa, lakini akafanywa hai katika
Roho. 19 [m]Baada ya kufanywa hai, alikwenda
na kuzihubiria roho zilizokuwa kifungoni:
20 [n]roho hizo ambazo zamani hazikutii,
wakati ule uvumilivu wa Mungu ulipokuwa
ukingoja katika siku za Noa, wakati wa
kujenga safina, ambamo watu wachache
tu, yaani watu wanane, waliokolewa ili
wasiangamie kwa gharika. 21 [o]Nayo maji
hayo ni kielelezo cha ubatizo ambao sasa
unawaokoa ninyi pia: si kwa kuondoa
uchafu kwenye mwili, bali kama ahadi
ya dhamiri safi kwa Mungu, kwa njia ya
ufufuo wa Yesu Kristo. 22 [p]Yeye ameingia
mbinguni na amekaa mkono wa kuume wa
Mungu; nao malaika, mamlaka na nguvu
zote wametiishwa chini yake.

### *Kuishi Kwa Ajili Ya Mungu*

4 [q]Kwa hiyo, kwa kuwa Kristo aliteswa
katika mwili wake, ninyi nanyi jivikeni
nia iyo hiyo kwa maana mtu aliyekwisha
kuteswa katika mwili ameachana na

---

[a]**3:7** Kol 3:19; 1Kor 7:3; Efe 5:25; Kol 3:10; 1Kor 12:23; 1The 4:14
[b]**3:8** Rum 12:10; Efe 4:2
[c]**3:9** Rum 12:17; 1The 5:15; 1Pet 2:21-23; Ebr 6:14
[d]**3:10** Za 34:12; Yak 1:26; 1Pet 2:1, 22; Ufu 14:5
[e]**3:11** Za 37:27; Isa 1:16, 17; 3Yn 11; Rum 12:8; 14:19
[f]**3:12** Za 34:12-16; Yn 9:31; Yak 5:16
[g]**3:13** Mit 16:7; Tit 2:14
[h]**3:14** 1Pet 4:15-16; Isa 8:12-14
[i]**3:15** Kol 4:6
[j]**3:16** Mdo 23:1; Ebr 13:18; 1Pet 2:12-15
[k]**3:17** 1Pet 4:19; 2:20; 4:15-16
[l]**3:18** 1Pet 2:21; Kol 1:22; 1Pet 4:1-6
[m]**3:19** 1Pet 1:12; 4:6; Isa 42:7; 49:9; 61:1
[n]**3:20** Mwa 6:3; Ebr 11:7
[o]**3:21** Mdo 22:16; Tit 3:5
[p]**3:22** Mk 16:19; Mt 28:18; Rum 8:38
[q]**4:1** 1Pet 3:18; Rum 6:2, 7; Gal 5:24; Kol 3:3, 5

dhambi. [2] [a]Kwa hivyo, haishi maisha yake
yaliyobaki ya kuishi hapa duniani kwa
tamaa mbaya za wanadamu, bali anaishi
kwa mapenzi ya Mungu. [3] [b]Maana wakati
uliopita mmekwisha kutumia muda wa
kutosha katika maisha yenu mkifanya
yale ambayo wapagani hupenda kutenda:
wakiishi katika uasherati, tamaa mbaya,
ulevi, karamu za ulafi, vileo, ngoma
mbaya, na ibada chukizo za sanamu. [4] [c]Wao
hushangaa kwamba ninyi hamjiingizi
pamoja nao katika huo wingi wa maisha
ya ufisadi, nao huwatukana ninyi. [5] [d]Lakini
itawapasa wao kutoa hesabu mbele zake
yeye aliye tayari kuwahukumu walio hai
na waliokufa. [6] [e]Kwa kuwa hii ndiyo sababu
Injili ilihubiriwa hata kwa wale waliokufa,
ili wahukumiwe sawasawa na wanadamu
wengine katika mwili, lakini katika roho
waishi kulingana na Mungu aishivyo.

[7] [f]Mwisho wa mambo yote umekaribia.
Kwa hiyo kuweni na akili tulivu na kiasi,
mkikesha katika kuomba. [8] [g]Zaidi ya
yote, dumuni katika upendo kwa maana
upendo husitiri wingi wa dhambi. [9] [h]Kuweni
wakarimu kila mtu na mwenzake pasipo
manung'uniko. [10] [i]Kila mmoja na atumie
kipawa chochote alichopewa kuwahudumia
wengine, kama mawakili waaminifu wa
neema mbalimbali za Mungu. [11] [j]Yeyote
asemaye hana budi kusema kama mtu
asemaye maneno ya Mungu mwenyewe.
Yeyote ahudumuye hana budi kuhudumu
kwa nguvu zile anazopewa na Mungu, ili
Mungu apate kutukuzwa katika mambo
yote kwa njia ya Yesu Kristo. Utukufu na
uweza una yeye milele na milele. Amen.

*Kuteseka Kwa Kuwa Mkristo*

[12] [k]Wapenzi, msione ajabu kwa yale
mateso yanayotukia miongoni mwenu,
kana kwamba ni kitu kigeni kinachowapata.
[13] [l]Bali furahini kuwa mnashiriki katika
mateso ya Kristo, ili mpate kufurahi zaidi
wakati utukufu wake utakapofunuliwa.
[14] [m]Kama mkitukanwa kwa ajili ya jina la
Kristo, mmebarikiwa, kwa sababu Roho wa
utukufu na wa Mungu anakaa juu yenu.
[15] [n]Lakini asiwepo mtu yeyote miongoni
mwenu anayeteswa kwa kuwa ni muuaji,
au mwizi, au mhalifu wa aina yoyote, au
anayejishughulisha na mambo ya watu
wengine. [16] [o]Lakini kama ukiteseka kwa
kuwa Mkristo, usihesabu jambo hilo kuwa
ni aibu, bali mtukuze Mungu kwa sababu
umeitwa kwa jina hilo. [17] [p]Kwa maana
wakati umewadia wa hukumu kuanzia
katika nyumba ya Mungu. Basi kama
ikianzia kwetu sisi, mwisho wa hao wasiotii
Injili ya Mungu utakuwaje? [18] [q]Basi,

"Ikiwa ni vigumu kwa mwenye haki
kuokoka,
itakuwaje kwa mtu asiyemcha
Mungu na mwenye dhambi?"

[19] [r]Kwa hiyo, wale wanaoteswa kulingana
na mapenzi ya Mungu, wajikabidhi kwa
Muumba wao aliye mwaminifu, huku
wakizidi kutenda mema.

*Kulichunga Kundi La Mungu*

5 [s]Kwa wazee waliomo miongoni mwenu,
nawasihi mimi nikiwa mzee mwenzenu,
shahidi wa mateso ya Kristo, na mshiriki
katika utukufu utakaofunuliwa: [2] [t]lichungeni
kundi la Mungu mlilokabidhiwa, mkitumika
kama waangalizi, si kwa kulazimishwa bali

---

[a]**4:2** Rum 6:2; 1Pet 1:14
[b]**4:3** Efe 2:2; Eze 44:6; 45:9; Mdo 17:30; Efe 4:17; 1The 4:15
[c]**4:4** 1Pet 3:16; Mdo 13:45; 18:6; 1Pet 3:16
[d]**4:5** Mdo 10:42; 2Tim 4:1
[e]**4:6** 1Pet 3:19
[f]**4:7** Rum 13:11; 1Pet 4:8
[g]**4:8** Ebr 13:1; Kol 3:14; Mit 10:12; 1Kor 13:7; Yak 5:20
[h]**4:9** Flp 2:14; 1Pet 4:10; Rum 12:6-7; 1Kor 4:2
[i]**4:10** Rum 12:6; 1Kor 4:7; Mt 24:45; Lk 12:42; 1Kor 4:1, 2
[j]**4:11** Efe 6:10; 1Kor 10:31
[k]**4:12** 1Pet 1:6-7; 1Kor 3:13
[l]**4:13** Rum 8:17; 1Pet 4:14; Mt 5:11
[m]**4:14** Mt 5:11; 2Kor 12:10; Yak 1:12; 1Pet 2:19, 20
[n]**4:15** Mdo 5:41; 1Pet 2:20; 1The 4:11; 1Tim 5:13
[o]**4:16** Mdo 5:41
[p]**4:17** Eze 9:6; 1Tim 3:15; 2The 1:8
[q]**4:18** Mit 11:31; Lk 23:31
[r]**4:19** Za 31:5; Lk 23:46; 2Tim 1:12
[s]**5:1** Mdo 11:30; Lk 24:48; 1Pet 4:13; Ufu 1:9
[t]**5:2** Yn 21:6; 1Tim 3:3

kwa hiari, kama Mungu anavyowataka mwe;
si kwa tamaa ya fedha, bali mlio na bidii
katika kutumika. 3 [a]Msijifanye mabwana juu
ya wale walio chini ya uangalizi wenu, bali
kuweni vielelezo kwa hilo kundi. 4 [b]Naye
Mchungaji Mkuu atakapodhihirishwa,
mtapokea taji ya utukufu isiyoharibika.
5 [c]Vivyo hivyo, ninyi mlio vijana watiini
wazee. Nanyi nyote imewapasa kujivika
unyenyekevu kila mtu kwa mwenzake, kwa
kuwa,

“Mungu huwapinga wenye kiburi,
lakini huwapa wanyenyekevu
neema.”

6 [d]Basi, nyenyekeeni chini ya mkono wa
Mungu ulio hodari, ili awakweze kwa
wakati wake. 7 [e]Mtwikeni yeye fadhaa zenu
zote, kwa maana yeye hujishughulisha sana
na mambo yenu.
8 [f]Mwe na kiasi na kukesha, maana adui
yenu ibilisi huzungukazunguka kama
simba angurumaye akitafuta mtu ili apate
kummeza. 9 [g]Mpingeni, mkiwa thabiti
katika imani, mkijua ya kwamba mateso
kama hayo yanawapata ndugu zenu pote
duniani.
10 [h]Nanyi mkiisha kuteswa kwa kitambo
kidogo, Mungu wa neema yote, aliyewaita
kuingia katika utukufu wake wa milele ndani
ya Kristo, yeye mwenyewe atawarejesha
na kuwatia nguvu, akiwaimarisha na
kuwathibitisha. 11 [i]Uweza una yeye milele
na milele. Amen.

*Salamu Za Mwisho*

12 [j]Kwa msaada wa Silvano,[k] ambaye
ninamhesabu kuwa ndugu mwaminifu,
nimewaandikia waraka huu mfupi ili
kuwatia moyo, na kushuhudia kwamba
hii ni neema halisi ya Mungu. Simameni
imara katika neema hiyo.
13 [l]Kanisa lililoko Babeli, lililochaguliwa
pamoja nanyi, wanawasalimu; vivyo
hivyo mwanangu Marko anawasalimu.
14 [m]Salimianeni kwa busu la upendo.
Amani iwe nanyi nyote mlio katika
Kristo.

---

[a]**5:3** Eze 34:4; Mt 20:25-28; Flp 3:17; 1Tim 4:12
[b]**5:4** 1Kor 9:25; Ebr 13:20; 1Kor 9:25; 2Tim 4:8; Yak 1:12; 1Pet 1:4
[c]**5:5** Efe 5:21; Mit 3:34; Yak 4:6
[d]**5:6** Yak 4:10
[e]**5:7** Mit 27:5; Mt 6:25; Ebr 13:5
[f]**5:8** Ay 1:7; Lk 21:34, 36; 1The 5:6; 1Pet 4:7; Ufu 12:12
[g]**5:9** Yak 4:7; Kol 2:5; Mdo 14:22
[h]**5:10** 2Kor 4:17; 2The 2:17
[i]**5:11** Rum 11:36; 1Pet 4:11; Ufu 1:6
[j]**5:12** 2Kor 1:19; Ebr 13:22
[k]12 Yaani Sila.
[l]**5:13** Mdo 12:12
[m]**5:14** Rum 16:16; Efe 6:23

# 2 PETRO

1 [a]Simoni Petro, mtumishi na mtume wa
Yesu Kristo:
Kwa wale ambao kwa njia ya haki ya
Mungu na Mwokozi wetu Yesu Kristo
mmepokea imani iliyo na thamani kama
yetu:
2 [b]Neema na amani iwe kwenu kwa wingi
katika kumjua Mungu na Yesu Bwana wetu.

*Wito Wa Mkristo Na Uteule*

3 [c]Uweza wake wa uungu umetupatia
mambo yote tunayohitaji kwa ajili ya
uzima na uchaji wa Mungu, kwa kumjua
yeye aliyetuita kwa utukufu wake na
wema wake mwenyewe. 4 [d]Kwa sababu
hiyo, ametukirimia ahadi zake kuu na za
thamani kupitia mambo haya, ili kupitia
hayo mpate kuwa washiriki wa asili ya
uungu, na kuokoka kutoka upotovu ulioko
duniani unaosababishwa na tamaa mbaya.
5 [e]Kwa sababu hii hasa, jitahidini sana
katika imani yenu kuongeza wema; na
katika wema, maarifa; 6 [f]katika maarifa,
kiasi; katika kiasi, saburi; katika saburi,
utauwa;[g] 7 [h]katika utauwa, upendano wa
ndugu; na katika upendano wa ndugu,
upendo. 8 [i]Kwa maana haya yakiwa ndani
yenu kwa wingi na kuzidi kuongezeka,
yanawasaidia msikose bidii wala kutozaa
matunda katika kumjua Bwana wetu Yesu
Kristo. 9 [j]Lakini mtu yeyote asipokuwa na
mambo haya haoni mbali, na ni kipofu,
naye amesahau kule kutakaswa kutoka
dhambi zake za zamani.
10 [k]Kwa hiyo, ndugu zangu, fanyeni
bidii zaidi kuuthibitisha wito wenu na
uteule wenu. Kwa maana mkifanya hivyo,
hamtajikwaa kamwe, 11 [l]na mtajaliwa kwa
ukarimu mwingi kuingia katika ufalme wa
milele wa Bwana na Mwokozi wetu Yesu
Kristo.

*Unabii Wa Maandiko*

12 [m]Hivyo nitawakumbusha mambo
haya siku zote, hata ingawa mnayajua na
mmethibitishwa katika kweli mliyo nayo.
13 [n]Naona ni vyema kuwakumbusha mambo
haya wakati wote niwapo katika hema hili
ambalo ni mwili wangu, 14 [o]kwa sababu
najua ya kwamba hivi karibuni nitaliweka
kando, kama vile Bwana wetu Yesu Kristo
alivyoliweka wazi kwangu. 15 [p]Nami
nitafanya kila juhudi kuona kwamba
baada ya kuondoka kwangu mtaweza
kuyakumbuka mambo haya siku zote.
16 [q]Tulipowafahamisha juu ya uweza
na kuja kwa Bwana wetu Yesu Kristo,
hatukufuata hadithi zilizotungwa kwa
werevu, bali tulishuhudia kwa macho yetu
ukuu wake. 17 Alipewa heshima na utukufu
kutoka kwa Mungu Baba, sauti ilipomjia
katika Utukufu Mkuu, ikisema, "Huyu
ni Mwanangu mpendwa. Ninapendezwa
naye sana." 18 Sisi wenyewe tuliisikia
sauti hii ambayo ilitoka mbinguni, wakati
tulipokuwa pamoja naye kwenye ule mlima
mtakatifu.
19 [r]Nasi tunalo pia neno la hakika
zaidi la unabii, ambalo mtafanya vyema
mkiliangalia kwa bidii, kama vile nuru

[a]**1:1** Rum 1:1; 1Pet 1:1; Rum 3:21-26; Tit 2:13
[b]**1:2** 2Pet 3:18; Rum 1:7; Flp 3:8; 2Pet 2:20; 1:3, 8
[c]**1:3** 1Pet 1:5; Rum 8:28; 1The 2:12
[d]**1:4** 2Kor 7:1; Efe 4:24; Ebr 12:10; Yak 1:27
[e]**1:5** Kol 2:3; 2Pet 3:18; 1Pet 3:7; Gal 5:6, 22; Yud 3
[f]**1:6** Mdo 24:25; Ebr 10:36; 2Pet 1:3
[g]6 Maana yake kumcha Mungu.
[h]**1:7** Rum 12:10; 1The 3:12; Gal 6:18; 1The 5:15; 1Yn 4:21
[i]**1:8** Yn 15:2; Kol 1:10
[j]**1:9** 1Yn 2:11; Mt 1:21
[k]**1:10** Za 15:5; Rum 8:28; Za 15:5; 2Pet 3:17; Yud 24
[l]**1:11** Za 145:13; 2Tim 4:18; 2Pet 2:20; 3:18
[m]**1:12** 1Yn 2:21; Flp 3:1; Yud 5; 2Yn 2
[n]**1:13** Isa 38:12; 2Kor 5:14; 2Pet 3:1; 2Kor 5:1, 4
[o]**1:14** 2Tim 4:6; Yn 13:36; 21:18, 19
[p]**1:15** Lk 9:31; Hes 22:4-20; 31:16; Kum 23:4; Yud 11; Ufu 2:14
[q]**1:16** Mk 13:26; Hes 22:21-30; 1Kor 1:17; 2:1, 4; 2Kor 2:17; 4:2
[r]**1:19** Za 119:105; Ufu 22:16

inavyong'aa gizani, hadi kupambazuka na
nyota ya asubuhi izuke mioyoni mwenu.
20 [a]Zaidi ya yote, yawapasa mjue kwamba
hakuna unabii katika Maandiko uliofasiriwa
kama alivyopenda nabii mwenyewe. 21 [b]Kwa
maana unabii haukuja kamwe kwa mapenzi
ya mwanadamu, bali watu walinena
yaliyotoka kwa Mungu wakiongozwa na
Roho Mtakatifu.

### *Walimu Wa Uongo Na Uangamivu Wao*

2 Lakini pia waliinuka manabii wa
uongo miongoni mwa watu, kama vile
watakavyokuwako walimu wa uongo
miongoni mwenu. Wataingiza mafundisho
yasiyopatana na kweli kwa siri, hata
kumkana Bwana wa pekee aliyewanunua,
na hivyo kujiletea wenyewe maangamizi
ya haraka. 2 Hata hivyo, wengi watafuata
njia zao za ufisadi, na kwa ajili yao njia
ya kweli itatukanwa. 3 [c]Nao katika tamaa
zao mbaya, walimu hawa watajipatia faida
kwenu kwa hadithi walizotunga wenyewe.
Lakini hukumu imekwisha kutangazwa
dhidi yao tangu zamani, wala uangamivu
wao haujalala usingizi.
4 [d]Kwa maana, kama Mungu
hakuwasamehe malaika walipotenda
dhambi, bali aliwatupa kuzimu[e] katika
vifungo vya giza wakae humo mpaka ije
hukumu; 5 [f]kama hakuusamehe ulimwengu
wa kale alipoleta gharika juu ya watu wale
wasiomcha Mungu, bali akamhifadhi Noa,
mhubiri wa haki, pamoja na watu wengine
saba; 6 [g]kama aliihukumu miji ya Sodoma
na Gomora kwa kuiteketeza kwa moto
ikawa majivu, na kuifanya kuwa kielelezo
kwa yale yatakayowapata wale wasiomcha
Mungu; 7 [h]na kama alimwokoa Loti, mtu
mwenye haki, ambaye alihuzunishwa na
maisha machafu ya watu wapotovu 8 [i](kwa
sababu yale matendo mapotovu aliyoyaona
na kuyasikia huyo mtu mwenye haki
alipoishi miongoni mwao yalimhuzunisha
siku baada ya siku): 9 [j]ikiwa hivyo ndivyo,
basi Bwana anajua jinsi ya kuwaokoa
wamchao Mungu kutoka majaribu, na
kuwaweka waasi katika adhabu hadi siku
ya hukumu. 10 [k]Hii ni hakika hasa kwa
wale wanaofuata tamaa mbaya za mwili
na kudharau mamlaka.
Kwa ushupavu na kwa kiburi, watu
hawa hawaogopi kunena mabaya dhidi
ya viumbe vya mbinguni. 11 Lakini hata
malaika, ingawa wana nguvu na uwezo
zaidi, hawaleti mashtaka mabaya dhidi ya
viumbe kama hao mbele za Bwana. 12 [l]Lakini
watu hawa hukufuru katika mambo
wasiyoyafahamu. Wao ni kama wanyama
wasio na akili, viumbe wanaotawaliwa na
hisia za mwili, waliozaliwa ili wakamatwe
na kuchinjwa. Hawa nao kama wanyama
wataangamizwa pia.
13 [m]Watalipwa madhara kwa ajili ya
madhara waliyowatendea wengine.
Huhesabu kuwa ni fahari kufanya karamu
za ulevi na ulafi mchana peupe. Wao ni
mawaa na dosari, wakijifurahisha katika
anasa zao wanaposhiriki katika karamu
zenu. 14 [n]Wakiwa na macho yaliyojaa
uzinzi, kamwe hawaachi kutenda dhambi.
Huwashawishi wale wasio imara. Wao
ni hodari kwa kutamani; ni wana wa
laana! 15 [o]Wameiacha njia iliyonyooka,
wakapotoka na kuifuata njia ya Balaamu
mwana wa Beori aliyependa mshahara wa
uovu. 16 [p]Lakini kwa ajili ya uovu wake,
alikemewa na punda, mnyama asiyejua
kusema, akaongea akitumia sauti ya

---

[a]**1:20** Rum 12:6; 2Pet 3:3
[b]**1:21** 2Tim 3:16; 2Sam 23:2; Mdo 1:16
[c]**2:3** 2Kor 2:17; 1The 2:5
[d]**2:4** 1Tim 3:6; Ufu 20:1, 2
[e]4 Kuzimu hapa linalotokana na neno Tartarus la Kiyunani; maana yake ni kule ndani sana katika mahali pa mateso kwa watu waliopotea.
[f]**2:5** 2Pet 3:6; Ebr 11:7; 1Pet 3:20
[g]**2:6** Mwa 19:24, 25
[h]**2:7** Mwa 19:16; 2Pet 3:17
[i]**2:8** Ebr 11:4; Eze 9:4; Za 119:130, 158
[j]**2:9** Za 37:33; 1Kor 10:13
[k]**2:10** 2Pet 3:3
[l]**2:12** Za 49:12
[m]**2:13** Isa 38:12; 2Kor 5:1, 4
[n]**2:14** 2Tim 4:6; Yn 13:36; 21:18, 19
[o]**2:15** Lk 9:31; Hes 22:4-20; 31:16; Kum 23:4; Yud 11; Ufu 2:14
[p]**2:16** Mk 13:26; Hes 22:21-30

mwanadamu na kuzuia wazimu wa huyo nabii.

17 [a]Watu hawa ni chemchemi zisizo na maji, na ukungu upeperushwao na tufani. Giza nene limewekwa tayari kwa ajili yao. 18 [b]Kwa maana wao hunena maneno makuu mno ya kiburi cha bure, na kwa kuvutia tamaa mbaya za asili ya mwili, huwashawishi watu ambao ndipo tu wamejiondoa miongoni mwa wale wanaoishi katika ufisadi. 19 [c]Huwaahidi uhuru hao waliowanasa, wakati wao wenyewe ni watumwa wa ufisadi: kwa maana mtu ni mtumwa wa kitu chochote kinachomtawala. 20 [d]Kama wameukimbia upotovu wa dunia kwa kumjua Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo, kisha wakanaswa tena humo na kushindwa, hali yao ya mwisho ni mbaya zaidi kuliko ile ya kwanza. 21 [e]Ingelikuwa afadhali kwao kama wasingeliijua kamwe njia ya haki, kuliko kuijua kisha wakaiacha ile amri takatifu waliyokabidhiwa. 22 [f]Imetukia kwao sawasawa na ile mithali ya kweli isemayo: “Mbwa huyarudia matapiko yake mwenyewe,” tena, “Nguruwe aliyeoshwa hurudi kugaagaa matopeni.”

*Ahadi Ya Kuja Kwa Bwana*

3 [g]Wapenzi, huu ndio waraka wangu wa pili ninaowaandikia. Katika nyaraka hizi mbili ninajaribu kuziamsha nia zenu safi kwa mawazo makamilifu. 2 [h]Nataka ninyi mkumbuke maneno yaliyosemwa zamani na manabii watakatifu na ile amri ya Bwana na Mwokozi mliyopewa kupitia kwa mitume wenu.

3 [i]Kwanza kabisa, ni lazima mfahamu ya kwamba siku za mwisho watakuja watu wenye dhihaka, wakidhihaki na kuzifuata tamaa zao mbaya. 4 [j]Watasema, “Iko wapi ile ahadi ya kuja kwake? Tangu baba zetu walipofariki, kila kitu kinaendelea kama kilivyokuwa tangu mwanzo wa kuumbwa.” 5 [k]Lakini wao kwa makusudi hupuuza ukweli huu, ya kwamba kwa neno la Mungu mbingu zilikuwepo tangu zamani, nayo dunia ilifanyizwa kutoka ndani ya maji na kwa maji. 6 [l]Ulimwengu wa wakati ule uligharikishwa kwa hayo maji na kuangamizwa. 7 [m]Lakini kwa neno lilo hilo, mbingu za sasa na dunia zimewekwa akiba kwa ajili ya moto, zikihifadhiwa hadi siku ile ya hukumu na ya kuangamizwa kwa watu wasiomcha Mungu.

8 [n]Lakini wapenzi, msisahau neno hili: kwamba kwa Bwana, siku moja ni kama miaka elfu, na miaka elfu ni kama siku moja. 9 [o]Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake, kama watu wengine wanavyokudhani kukawia. Badala yake, yeye anawavumilia ninyi, maana hataki mtu yeyote aangamie, bali kila mtu afikilie toba.

10 [p]Lakini siku ya Bwana itakuja kama mwizi. Ndipo mbingu zitatoweka kwa kishindo kikuu; navyo vitu vya asili vitateketezwa kwa moto, nayo dunia na kila kitu kilichomo ndani yake kitaunguzwa.

11 [q]Kwa kuwa vitu vyote vitaharibiwa namna hii, je, ninyi imewapasa kuwa watu wa namna gani? Inawapasa kuishi maisha matakatifu na ya kumcha Mungu, 12 [r]mkingojea na kuhimiza kuja kwa hiyo siku ya Mungu. Siku hiyo italeta mbingu kuchomwa moto na kutoweka, na vitu vya asili vitayeyuka kwa moto. 13 [s]Lakini kufuatana na ahadi yake, sisi tunatazamia mbingu mpya na dunia mpya, ambayo haki hukaa ndani yake.

[a]**2:17** Mt 3:17; Yud 12, 13
[b]**2:18** Mt 17:6; Yud 16; 2Pet 2:20; 1:4
[c]**2:19** Za 119:105; Ufu 22:16
[d]**2:20** 2Tim 3:16; 2Sam 23:2
[e]**2:21** Eze 18:24; Ebr 10:26, 27
[f]**2:22** Mit 26:11
[g]**3:1** 2Pet 1:13; 1Kor 10:14
[h]**3:2** 1Tim 4:1; Yud 18; Lk 1:70; Mdo 3:21; Efe 4:11
[i]**3:3** 1Tim 4:1; 2Tim 3:1; 2Pet 2:10
[j]**3:4** Isa 5:19; Lk 17:30; Mk 10:6
[k]**3:5** Mwa 1:6, 9; Ebr 11:1; Za 24:2
[l]**3:6** Mwa 7:21, 22; 2Pet 2:5
[m]**3:7** 2The 1:7; 2Pet 3:10; Mt 25:41; 2The 1:8
[n]**3:8** Za 90:4
[o]**3:9** Hab 2:3; Ebr 10:37; Rum 2:11; 1Tim 2:4; Ufu 2:21
[p]**3:10** Lk 12:39; 1The 5:2; Ebr 12:27; Ufu 21:11
[q]**3:11** 1Pet 1:15
[r]**3:12** 1Kor 1:7; Za 50:3
[s]**3:13** Isa 66:22; Ufu 21:1

14 [a]Kwa sababu hii, wapenzi, kwa kuwa
mnatazamia mambo haya, fanyeni bidii ili
awakute katika amani, bila mawaa wala
dosari. 15 [b]Hesabuni uvumilivu wa Bwana
kuwa ni wokovu, kama vile ndugu yetu
mpenzi Paulo alivyowaandikia kwa hekima
ile aliyopewa na Mungu. 16 [c]Huandika
vivyo hivyo katika nyaraka zake zote,
akizungumzia ndani yake mambo haya.
Katika nyaraka zake kuna mambo mengine
ambayo ni vigumu kuyaelewa, ambayo
watu wajinga na wasio thabiti huyapotosha
kwa maangamizi yao wenyewe, kama
wapotoshavyo pia Maandiko mengine.

17 [d]Basi, ninyi wapenzi, kwa kuwa
mmekwisha kujua mambo haya, jilindeni
msije mkachukuliwa na kosa la watu hao
waasi na kuanguka kutoka kwenye uthabiti
wenu. 18 [e]Bali kueni katika neema na katika
kumjua Bwana na Mwokozi wetu Yesu
Kristo. Utukufu una yeye sasa na milele!
Amen.

---

[a]**3:14** 1Kor 1:7, 8; Yud 24; 1The 3:13
[b]**3:15** Rum 2:4; Efe 3:3; 2Pet 3:9; 1Pet 3:20
[c]**3:16** Yak 1:8; 2Pet 2:14
[d]**3:17** 1Kor 10:12; 2Pet 2:18; Ufu 2:5
[e]**3:18** 2Pet 1:11; 2:20

# 1 YOHANA

*Neno La Uzima*

1 [a]Tunawajulisha lile lililokuwepo
tangu mwanzo, lile tulilosikia, ambalo
tumeliona kwa macho yetu, ambalo
tumelitazama na kuligusa kwa mikono
yetu, kuhusu Neno la uzima. 2 [b]Uzima
huo ulidhihirishwa; nasi tumeuona na
kuushuhudia, nasi twawatangazia uzima wa
milele, ambao ulikuwa pamoja na Baba, nao
ukadhihirishwa kwetu. 3 [c]Twawatangazia
lile tuliloliona na kulisikia, ili nanyi mwe
na ushirika nasi. Na ushirika wetu hasa ni
pamoja na Baba na Mwanawe, Yesu Kristo.
4 Tunaandika mambo haya ili furaha yetu
ipate kuwa timilifu.

*Kutembea Nuruni*

5 [d]Huu ndio ujumbe tuliosikia kutoka
kwake na kuwatangazia ninyi: kwamba
Mungu ni nuru na ndani yake hamna
giza lolote. 6 [e]Kama tukisema kwamba
twashirikiana naye huku tukienenda gizani,
twasema uongo, wala hatutendi lililo kweli.
7 [f]Lakini tukienenda nuruni, kama yeye
alivyo nuruni, twashirikiana sisi kwa sisi na
damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha
dhambi yote.
8 [g]Kama tukisema kwamba hatuna dhambi,
twajidanganya wenyewe wala kweli haimo
ndani yetu. 9 [h]Kama tukiziungama dhambi
zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki,
atatusamehe dhambi zetu na kutusafisha
kutoka kwenye udhalimu wote. 10 [i]Kama
tukisema hatukutenda dhambi, twamfanya
yeye kuwa mwongo na neno lake halimo
ndani yetu.

*Kristo Mwombezi Wetu*

2 [j]Watoto wangu wapendwa, nawaandikia
haya ili msitende dhambi. Lakini kama
mtu yeyote akitenda dhambi, tunaye
Mwombezi kwa Baba: ndiye Yesu Kristo,
Mwenye Haki. 2 [k]Yeye ndiye dhabihu ya
upatanisho kwa ajili ya dhambi zetu, wala
si kwa ajili ya dhambi zetu tu, bali pia kwa
ajili ya dhambi za ulimwengu wote.
3 [l]Basi katika hili twajua ya kuwa
tumemjua, tukizishika amri zake. 4 [m]Mtu
yeyote asemaye kuwa, "Ninamjua," lakini
hazishiki amri zake, ni mwongo, wala
ndani ya mtu huyo hamna kweli. 5 [n]Lakini
mtu yeyote anayelitii neno lake, upendo
wa Mungu umekamilika ndani yake kweli
kweli. Katika hili twajua kuwa tumo ndani
yake. 6 [o]Yeyote anayesema anakaa ndani
yake hana budi kuenenda kama Yesu
alivyoenenda.

*Amri Mpya*

7 [p]Wapendwa, siwaandikii ninyi amri
mpya bali ile ya zamani, ambayo mmekuwa
nayo tangu mwanzo. Amri hii ya zamani ni
lile neno mlilosikia. 8 [q]Lakini nawaandikia
amri mpya, yaani, lile neno lililo kweli
ndani yake na ndani yenu, kwa sababu giza
linapita na ile nuru ya kweli tayari inang'aa.
9 [r]Yeyote anayesema yumo nuruni lakini
anamchukia ndugu yake bado yuko gizani.

---

[a]**1:1** Yn 1:2; 2Pet 1:16; Yn 20:27
[b]**1:2** Yn 14:6; 1Pet 1:20
[c]**1:3** 1Kor 1:9; 1Yn 1:1; Mdo 4:20; Yn 17:21; 1Yn 2:24
[d]**1:5** 1Yn 3:11; 2Yn 12
[e]**1:6** Efe 5:8; 1Yn 4:20
[f]**1:7** Ufu 7:14; Ebr 9:14; Ufu 1:5
[g]**1:8** Yer 2:35; Yn 8:44
[h]**1:9** Mit 28; 13; Za 32:5; 51:2; Mit 28:13; 1Yn 1:7; Mik 7:18-20; Ebr 10:22
[i]**1:10** 1Yn 5:10; Yn 5:38; 1Yn 1:8; 5:10; Yn 5:38; 2:15
[j]**2:1** 1The 2:11; Ebr 7:25; 1Tim 2:5
[k]**2:2** 1Yn 4:10; Rum 3:25; Mt 1:21; Yn 3:17
[l]**2:3** Yn 14:15; 1Yn 2:5; 3:24; 4:13; 5:2; 2:4
[m]**2:4** 1Yn 1:6, 8; 2:3; Tit 1:16; 1Yn 3:6; 4:7, 8
[n]**2:5** Yn 14:15, 21, 23; 1Yn 4:12
[o]**2:6** Mt 11:29; 2Pet 2:21
[p]**2:7** 1Kor 10:14; 1Yn 2:24; 3:11, 23; 4:2
[q]**2:8** Yn 13:34; Ebr 10:25; Yn 1:9; Efe 5:8; 1The 5:5
[r]**2:9** 1Yn 2:11; Law 19:17; 1Yn 3:10; 4:20, 21; 1:5

10 [a]Yeye ampendaye ndugu yake anakaa
nuruni, wala hakuna kitu chochote ndani
yake cha kumkwaza. 11 [b]Lakini yeyote
amchukiaye ndugu yake, yuko gizani na
anaenenda gizani, wala hajui anakokwenda,
kwa sababu giza limempofusha macho.

12 [c]Nawaandikia ninyi, watoto wadogo,
kwa sababu dhambi zenu
zimesamehewa kwa ajili ya Jina lake.
13 [d]Nawaandikia ninyi, akina baba,
kwa sababu mmemjua
yeye aliye tangu mwanzo.
Nawaandikia ninyi vijana
kwa sababu mmemshinda yule mwovu.
Nawaandikia ninyi watoto wadogo,
kwa sababu mmemjua Baba.
14 [e]Nawaandikia ninyi akina baba,
kwa sababu mmemjua
yeye aliye tangu mwanzo.
Nawaandikia ninyi vijana,
kwa sababu mna nguvu,
na neno la Mungu linakaa ndani yenu,
nanyi mmemshinda yule mwovu.

*Msiupende Ulimwengu*

15 [f]Msiupende ulimwengu wala mambo
yaliyo ulimwenguni. Kama mtu yeyote
akiupenda ulimwengu, upendo wa Baba
haumo ndani yake. 16 [g]Kwa maana kila
kitu kilichomo ulimwenguni, yaani tamaa
ya mwili, tamaa ya macho na kiburi cha
uzima, havitokani na Baba bali hutokana
na ulimwengu. 17 [h]Nao ulimwengu unapita,
pamoja na tamaa zake, bali yeye afanyaye
mapenzi ya Mungu adumu milele.

*Onyo Dhidi Ya Wapinga Kristo*

18 [i]Watoto wadogo, huu ni wakati wa
mwisho! Kama mlivyosikia kwamba mpinga
Kristo anakuja, hivyo basi wapinga Kristo
wengi wamekwisha kuja. Kutokana na hili
twajua kwamba huu ni wakati wa mwisho.
19 [j]Walitoka kwetu, lakini hawakuwa wa
kwetu hasa. Kwa maana kama wangelikuwa
wa kwetu, wangelikaa pamoja nasi, lakini
kutoka kwao kulionyesha kwamba hakuna
hata mmoja wao aliyekuwa wa kwetu.
20 [k]Lakini ninyi mmetiwa mafuta na yeye
Aliye Mtakatifu, nanyi nyote mnaijua kweli.
21 [l]Siwaandikii kwa sababu hamuijui kweli,
bali kwa sababu mnaijua, nanyi mnajua
hakuna uongo utokao katika kweli. 22 [m]Je,
mwongo ni nani? Mwongo ni mtu yule
asemaye kwamba Yesu si Kristo. Mtu wa
namna hiyo ndiye mpinga Kristo, yaani,
yeye humkana Baba na Mwana. 23 [n]Hakuna
yeyote amkanaye Mwana aliye na Baba.
Yeyote anayemkubali Mwana anaye na
Baba pia.
24 [o]Hakikisheni kwamba lile mlilosikia
tangu mwanzo linakaa ndani yenu. Kama
lile mlilosikia tangu mwanzo linakaa ndani
yenu, ninyi nanyi mtakaa ndani ya Mwana
na ndani ya Baba. 25 [p]Hii ndiyo ahadi yake
kwetu, yaani, uzima wa milele.
26 [q]Nawaandikia mambo haya kuhusu
wale watu ambao wanajaribu kuwapotosha.
27 [r]Nanyi, upako mlioupata kutoka kwake
unakaa ndani yenu, wala ninyi hamna haja
ya mtu yeyote kuwafundisha. Lakini kama
vile upako wake unavyowafundisha kuhusu
mambo yote nayo ni kweli wala si uongo,
basi kama ulivyowafundisha kaeni ndani
yake.

---

[a]**2:10** 1Yn 3:14; 2:11; Za 119:165; Rum 14:13, 15; Yn 11:9
[b]**2:11** Yn 11:9; 11:10; 12:35; 1Yn 1:6; Yn 12:35
[c]**2:12** 1Yn 2:9; 3:23
[d]**2:13** Mt 5:37; Yn 1:1; 16:33; 1Yn 2:14; 2:13
[e]**2:14** Efe 6:10; Yn 5:38; 1Yn 1:10
[f]**2:15** Rum 12:2; Yak 4:4
[g]**2:16** Efe 2:8; Mit 27:20
[h]**2:17** Ebr 12:27; Mt 12:50; 1Kor 7:31; Yak 1:10; 4:14; 1Pet 1:24
[i]**2:18** 1Yn 4:1; 2Yn 7
[j]**2:19** Mk 1:24; Yer 31:34
[k]**2:20** 1Yn 2:27; 2Kor 1:21; Mk 1:24; Yer 31:34; Mt 13:11; Yn 14:26
[l]**2:21** 2Pet 1:12; Yud 5
[m]**2:22** 1Yn 4:13; 2Yn 7
[n]**2:23** Yn 14:7; 2Yn 9
[o]**2:24** 2Yn 9
[p]**2:25** Mt 25:46; Yn 17:3; 1Yn 1:2; 5:11
[q]**2:26** 1Yn 3:7; 2Yn 7
[r]**2:27** 1Yn 2:20; Yer 31:33, 34; Ebr 8:10, 11; Yn 14:26; 16:13

*Watoto Wa Mungu*

28 [a]Sasa basi, watoto wapendwa, kaeni
ndani yake, ili atakapofunuliwa, tuwe na
ujasiri, wala tusiaibike mbele zake wakati
wa kuja kwake.
29 [b]Kama mkijua kuwa yeye ni mwenye
haki, mwajua kwamba kila atendaye haki
amezaliwa naye.
3 [c]Tazameni ni pendo kuu namna gani
alilotupa Baba, kwamba sisi tuitwe wana
wa Mungu! Na ndivyo tulivyo. Kwa sababu
hii ulimwengu hautambui, kwa kuwa
haukumtambua yeye. 2 [d]Wapendwa, sasa tu
wana wa Mungu, lakini bado haijadhihirika
tutakavyokuwa, lakini twajua ya kwamba
yeye atakapodhihirishwa, tutafanana naye,
kwa maana tutamwona kama alivyo. 3 [e]Kila
mmoja mwenye matumaini haya ndani yake
hujitakasa, kama vile yeye alivyo mtakatifu.
4 [f]Kila mtu atendaye dhambi afanya
uasi, kwa kuwa dhambi ni uasi. 5 [g]Lakini
mwajua ya kuwa yeye alidhihirishwa ili
aziondoe dhambi, wala ndani yake hamna
dhambi. 6 [h]Kila mtu akaaye ndani yake
hatendi dhambi. Kila mtu atendaye dhambi
hakumwona yeye wala hakumtambua.
7 [i]Watoto wapendwa, mtu yeyote
asiwadanganye. Kila mtu atendaye haki
ana haki, kama yeye alivyo na haki.
8 [j]Yeye atendaye dhambi ni wa ibilisi, kwa
sababu ibilisi amekuwa akitenda dhambi
tangu mwanzo. Kwa kusudi hili Mwana
wa Mungu alidhihirishwa, ili aziangamize
kazi za ibilisi. 9 [k]Yeyote aliyezaliwa na
Mungu hatendi dhambi, kwa sababu uzao
wa Mungu wakaa ndani yake, wala hawezi
kutenda dhambi kwa sababu amezaliwa
na Mungu. 10 [l]Kwa jinsi hii tunaweza kujua
dhahiri watoto wa Mungu na pia watoto
wa ibilisi. Yeyote asiyetenda haki hatokani
na Mungu, wala yeye asiyempenda ndugu
yake.

*Mpendane Ninyi Kwa Ninyi*

11 [m]Hili ndilo neno mlilolisikia tangu
mwanzo: Kwamba imetupasa tupendane sisi
kwa sisi. 12 [n]Msiwe kama Kaini aliyekuwa wa
yule mwovu akamuua ndugu yake. Basi kwa
nini alimuua? Ni kwa sababu matendo yake
Kaini yalikuwa mabaya na ya ndugu yake
yalikuwa ya haki. 13 [o]Ndugu zangu, ninyi
msistaajabu kama ulimwengu ukiwachukia.
14 [p]Sisi tunajua ya kwamba tumepita mautini
kuingia uzimani, kwa sababu tunawapenda
ndugu. Kila asiyempenda ndugu yake akaa
mautini. 15 [q]Yeyote amchukiaye ndugu
yake ni muuaji, nanyi mwajua ya kwamba
muuaji hana uzima wa milele ndani yake.
16 [r]Kwa namna hii twaweza kulijua pendo
la Mungu: Kwa sababu Yesu Kristo aliutoa
uhai wake kwa ajili yetu. Nasi imetupasa
kuutoa uhai kwa ajili ya hao ndugu. 17 [s]Ikiwa
mtu anavyo vitu vya ulimwengu huu na
akamwona ndugu yake ni mhitaji lakini
asimhurumie, upendo wa Mungu wakaaje
ndani ya mtu huyo? 18 [t]Watoto wapendwa,
tusipende kwa maneno au kwa ulimi bali
kwa tendo na kweli. 19 [u]Basi hivi ndivyo
tutakavyoweza kujua ya kuwa sisi tu wa
kweli na hivyo twaithibitisha mioyo yetu
mbele za Mungu 20 [v]kila mara mioyo yetu
inapotuhukumu. Kwa maana Mungu ni
mkuu kuliko mioyo yetu, naye anajua kila
kitu.
21 [w]Wapendwa, kama mioyo yetu

[a]**2:28** Kol 3:4; 1Yn 3:2; Efe 3:12; 1The 2:19
[b]**2:29** 1Yn 3:7; Mdo 22:14; Yn 1:13
[c]**3:1** Yn 3:16; 15:21
[d]**3:2** Rum 8:29; 2Pet 1:4; Za 17:15
[e]**3:3** 2Kor 7:1; 2Pet 3:13, 14
[f]**3:4** 1Yn 5:17; Mt 7:23; Rum 4:15
[g]**3:5** 2Kor 5:21; 1Yn 1:2; Isa 53:5, 6, 11; 1Tim 1:15; Ebr 1:3; 9:26; 1Pet 2:24
[h]**3:6** 1Yn 5:18; 3Yn 1; 1Yn 2:4
[i]**3:7** 1Yn 2:1; 2:26; 2:29
[j]**3:8** Yn 1:13; Za 119:3; 1Pet 1:23
[k]**3:9** Yn 1:13; 1Yn 3:6; Za 119:3; 1Yn 5:18; 1Pet 1:23
[l]**3:10** 1Yn 3:1, 2; Yn 1:12; 1Yn 3:8; 4:8; 2:9
[m]**3:11** 1Yn 1:5; Yn 15:12
[n]**3:12** Mwa 4:8; Mt 5:37; Za 38:20; Mit 29:10
[o]**3:13** Yn 15:18, 19; 17:14
[p]**3:14** Yn 5:24; 1Yn 2:9
[q]**3:15** Mt 5:21, 22; Gal 5:20, 21; Yn 3:16
[r]**3:16** Yn 10:11; 15:13; Flp 2:17; 1The 2:8
[s]**3:17** Yak 2:15, 16; 1Yn 4:20
[t]**3:18** 1Yn 2:1; Eze 33:1; Rum 12:9
[u]**3:19** Yn 18:37; 1Yn 1:8
[v]**3:20** 1Kor 4:4
[w]**3:21** Efe 3:12; 1Kor 10:14; 1Yn 5:14

haituhukumu, tunao ujasiri mbele za Mungu, 22 [a]lolote tuombalo, twalipokea kutoka kwake, kwa sababu tumezitii amri zake na kutenda yale yanayompendeza. 23 [b]Hii ndiyo amri yake: kwamba tuliamini Jina la Mwanawe, Yesu Kristo, na kupendana sisi kwa sisi kama yeye alivyotuamuru. 24 [c]Wale wote wanaozishika amri zake hukaa ndani yake na yeye ndani yao. Hivi ndivyo tunavyojua kwamba anakaa ndani yetu. Nasi twajua hili kwa njia ya Roho yule aliyetupa.

### *Zijaribuni Hizo Roho*

4 [d]Wapendwa, msiamini kila roho, bali zijaribuni hizo roho mwone kama zimetoka kwa Mungu, kwa sababu manabii wengi wa uongo wametokea ulimwenguni. 2 [e]Hivi ndivyo mnavyoweza kutambua Roho wa Mungu: Kila roho inayokubali kwamba Yesu Kristo amekuja katika mwili yatoka kwa Mungu. 3 [f]Lakini kila roho ambayo haimkubali Yesu haitoki kwa Mungu. Hii ndiyo roho ya mpinga Kristo, ambayo mmesikia kwamba inakuja na sasa tayari iko ulimwenguni.

4 [g]Watoto wapendwa, ninyi mmetokana na Mungu, nanyi mmewashinda kwa sababu yeye aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye aliye katika ulimwengu. 5 [h]Wao wanatokana na ulimwengu na kwa hiyo hunena yaliyo ya ulimwengu, hivyo ulimwengu huwasikiliza. 6 [i]Sisi twatokana na Mungu na yeyote anayemjua Mungu hutusikiliza, lakini asiyetokana na Mungu hatusikilizi. Hivi ndivyo tunavyoweza kutambua Roho wa Kweli na roho ya upotovu.

### *Mungu Ni Pendo*

7 [j]Wapendwa, tupendane, kwa kuwa pendo latoka kwa Mungu. Kila apendaye amezaliwa na Mungu, naye anamjua Mungu. 8 [k]Yeye asiyependa hamjui Mungu, kwa sababu Mungu ni pendo. 9 [l]Hivi ndivyo Mungu alivyoonyesha pendo lake kwetu: Mungu alimtuma Mwanawe wa pekee ulimwenguni, ili tupate uzima kupitia kwake. 10 [m]Hili ndilo pendo: si kwamba tulimpenda Mungu, bali yeye alitupenda, akamtuma Mwanawe, ili yeye awe dhabihu ya upatanisho kwa ajili ya dhambi zetu. 11 [n]Marafiki wapendwa, kama Mungu alivyotupenda sisi, imetupasa na sisi kupendana. 12 [o]Hakuna mtu yeyote aliyemwona Mungu wakati wowote. Lakini tukipendana, Mungu anakaa ndani yetu, na pendo lake limekamilika ndani yetu.

13 [p]Tunajua kwamba twakaa ndani yake na yeye ndani yetu, kwa sababu ametupa sisi sehemu ya Roho wake. 14 [q]Nasi tumeona na kushuhudia kwamba Baba amemtuma Mwanawe ili awe Mwokozi wa ulimwengu. 15 [r]Kila akiriye kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu, basi Mungu hukaa ndani yake, naye ndani ya Mungu. 16 [s]Hivyo nasi twajua na kulitumainia pendo la Mungu alilo nalo kwa ajili yetu.

Mungu ni Upendo. Kila akaaye katika upendo hukaa ndani ya Mungu na Mungu hukaa ndani yake. 17 [t]Kwa njia hii, pendo hukamilishwa miongoni mwetu ili tupate kuwa na ujasiri katika siku ya hukumu, kwa sababu kama alivyo ndivyo tulivyo sisi katika ulimwengu huu. 18 [u]Katika pendo hakuna hofu. Lakini pendo lililo kamili huitupa nje hofu, kwa sababu hofu

[a]**3:22** Mt 7:7; Ebr 13:21
[b]**3:23** Yn 6:23; 13:34
[c]**3:24** 1Yn 4:15; 1The 4:8
[d]**4:1** Mt 7:15; 1Kor 10:14; Yer 29:9; 1Kor 12:10; 2The 2:2; 1Yn 2:18
[e]**4:2** Yn 1:4; 1Yn 2:23; 1Kor 12:3
[f]**4:3** 1Yn 2:22; 2Yn 7; 1Yn 2:18
[g]**4:4** Rum 8:31; 2Fal 6:16
[h]**4:5** Yn 17:14, 16
[i]**4:6** Yn 8:47; 14:17
[j]**4:7** 1Yn 3:11; 2:4
[k]**4:8** 1Yn 4:7, 16; 2:4; 3:6
[l]**4:9** Yn 3:16; 17; 1Yn 5:11
[m]**4:10** Rum 5:8, 10; 1Yn 2:2
[n]**4:11** Yak 3:16; 1Yn 2:25; Yn 1:4; 1Yn 4:9
[o]**4:12** Yn 1:18; 1Tim 6:16
[p]**4:13** 1Yn 3:24; 2:3
[q]**4:14** Yn 15:27; Lk 2:10
[r]**4:15** 1Yn 5:5; Rum 10:9
[s]**4:16** 1Yn 4:8, 12, 13; 3:24
[t]**4:17** 1Yn 4:12; 2:5; Efe 3:12; Mt 10:15
[u]**4:18** Rum 8:15; 1Yn 4:12

inahusika na adhabu. Kila mwenye hofu hakukamilika katika pendo.

19 [a]Twampenda yeye kwa sababu yeye alitupenda kwanza. 20 [b]Ikiwa mtu atasema, “Nampenda Mungu,” lakini anamchukia ndugu yake, yeye ni mwongo. Kwa maana kila mtu asiyempenda ndugu yake ambaye anamwona, atampendaje Mungu asiyemuona? 21 Naye ametupa amri hii: Yeyote anayempenda Mungu lazima pia ampende ndugu yake.

### *Imani Katika Mwana Wa Mungu Huushinda Ulimwengu*

5 [c]Kila mtu anayeamini kwamba Yesu ndiye Kristo amezaliwa na Mungu, na yeyote ampendaye Baba humpenda pia mtoto aliyezaliwa naye. 2 [d]Hivi ndivyo tunavyojua kwamba tunawapenda watoto wa Mungu, kwa kumpenda Mungu na kuzitii amri zake. 3 [e]Huku ndiko kumpenda Mungu, yaani, kuzitii amri zake. Nazo amri zake si nzito. 4 [f]Kwa maana kila aliyezaliwa na Mungu huushinda ulimwengu. Huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu, yaani, hiyo imani yetu. 5 [g]Ni nani yule aushindaye ulimwengu? Ni yule tu aaminiye kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu.

### *Ushuhuda Kuhusu Mwana Wa Mungu*

6 [h]Huyu ndiye alikuja kwa maji na damu, yaani, Yesu Kristo. Hakuja kwa maji peke yake, bali kwa maji na damu. Naye Roho ndiye ashuhudiaye, kwa sababu Roho ndiye kweli. 7 [i]Kwa maana wako watatu washuhudiao[ mbinguni: hao ni Baba, Neno na Roho Mtakatifu. Hawa watatu ni umoja. 8 Pia wako mashahidi watatu duniani]: Roho, Maji na Damu; hawa watatu wanakubaliana katika umoja. 9 [j]Kama tunaukubali ushuhuda wa wanadamu, basi ushuhuda wa Mungu ni mkuu zaidi, kwa kuwa huu ndio ushuhuda wa Mungu kwamba amemshuhudia Mwanawe. 10 [k]Kila mtu amwaminiye Mwana wa Mungu anao huu ushuhuda moyoni mwake. Kila mtu asiyemwamini Mungu amemfanya yeye kuwa mwongo, kwa sababu hakuamini ushuhuda Mungu alioutoa kuhusu Mwanawe. 11 [l]Huu ndio ushuhuda: kwamba Mungu ametupa uzima wa milele, nao huo uzima umo katika Mwanawe. 12 [m]Aliye naye Mwana wa Mungu anao uzima, yeye asiye na Mwana wa Mungu hana uzima.

### *Maneno Ya Mwisho*

13 [n]Nawaandikia mambo haya ninyi mnaoliamini Jina la Mwana wa Mungu ili mpate kujua ya kuwa mnao uzima wa milele. 14 [o]Huu ndio ujasiri tulio nao tunapomkaribia Mungu, kwamba kama tukiomba kitu sawasawa na mapenzi yake, atusikia. 15 [p]Nasi kama tunajua atusikia, lolote tuombalo, tunajua ya kwamba tumekwisha kupata zile haja tulizomwomba.

16 [q]Kama mtu akimwona ndugu yake akitenda dhambi isiyo ya mauti, inampasa aombe, naye Mungu atampa uzima mtu huyo. Ninamaanisha wale ambao dhambi yao si ya mauti. Iko dhambi ya mauti, sisemi kwamba utaomba kwa ajili ya hiyo. 17 [r]Jambo lolote lisilo la haki ni dhambi, lakini iko dhambi isiyo ya mauti.

18 [s]Tunajua ya kuwa yeye aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi, bali aliyezaliwa na Mungu hujilinda, wala yule mwovu hawezi

---

[a]**4:19** 1Yn 4:10
[b]**4:20** 1Yn 2:9; 3:17; Yn 1:18
[c]**5:1** Yn 3:15; 1Yn 2:22; 2:23; Yn 8:42
[d]**5:2** 1Yn 2:3; 3:14
[e]**5:3** Yn 14:15; Mt 11:30; 23:4
[f]**5:4** Yn 1:13; 16:33
[g]**5:5** 1Yn 2:23
[h]**5:6** Yn 19:34; 14:17
[i]**5:7** Mt 18:16
[j]**5:9** Yn 5:34; Mt 3:16, 17; Yn 5:32, 37; 8:15, 18
[k]**5:10** Rum 8:16; Gal 4:6; Yn 3:33; 1Yn 1:10
[l]**5:11** Mt 25:46; Yn 1:4
[m]**5:12** Yn 3:15, 16, 36
[n]**5:13** Yn 3:23; 1Yn 5:11; Mt 25:46
[o]**5:14** Efe 3:12; 1Yn 3:21; Mt 7:7
[p]**5:15** 1Yn 5:18, 20; 1Fal 3:12
[q]**5:16** Yak 5:15; Kut 23:21; Ebr 6:4-6; 10:26; Yer 7:16; 14:11
[r]**5:17** 1Yn 3:4; 5:16; 2:1
[s]**5:18** Yn 1:13; Mt 5:37; 14:30

kumdhuru. 19 [a]Sisi twajua kuwa tu watoto
wa Mungu na ya kwamba ulimwengu wote
uko chini ya utawala wa yule mwovu.
20 [b]Nasi pia twajua ya kwamba Mwana
wa Mungu amekuja, naye ametupa sisi
ufahamu ili tupate kumjua yeye aliye Kweli.
Nasi tumo ndani yake yeye aliye Kweli,
yaani, ndani ya Yesu Kristo Mwanawe. Yeye
ndiye Mungu wa kweli na uzima wa milele.
21 [c]Watoto wapendwa, jilindeni nafsi
zenu kutokana na sanamu. Amen.

---

[a]**5:19** 1Yn 4:6; Yn 12:31; 14:30; 17:15
[b]**5:20** 1Yn 5:5; Lk 24:45; Yn 17:3; 1Yn 5:11; Mt 25:46
[c]**5:21** 1Yn 2:1; 1Kor 10:14; 1The 1:9

# 2 YOHANA

*Salamu*

1 [a]Mzee:
Kwa bibi mteule na watoto wake,
niwapendao katika kweli, wala si mimi tu,
bali na wale wote waijuayo kweli: 2 [b]kwa
sababu ya ile kweli ikaayo ndani yetu na
ambayo itaendelea kukaa nasi milele:
3 [c]Neema, rehema na amani itokayo kwa
Mungu Baba na kwa Yesu Kristo, Mwanawe
Baba, itakuwa pamoja nasi katika kweli
na upendo.

*Kweli Na Upendo*

4 Imenipa furaha kuu kuona baadhi ya
watoto wako wanaenenda katika kweli,
kama vile Baba alivyotuagiza. 5 [d]Sasa,
bibi mpendwa, si kwamba ninakuandikia
amri mpya, bali ile tuliyokuwa nayo
tangu mwanzo. Tupendane kila mmoja na
mwenzake. 6 [e]Hili ndilo pendo, kwamba
tuenende sawasawa na amri zake. Hii
ndiyo amri yake kama vile mlivyosikia
tangu mwanzo, kwamba mwenende katika
upendo.
7 [f]Wadanganyifu wengi, wasiokubali
kwamba Yesu Kristo amekuja katika
mwili, wametokea ulimwenguni. Mtu wa
namna hiyo ni mdanganyifu na mpinga
Kristo. 8 [g]Jihadharini msije mkapoteza kile
mlichokitenda, bali mpate kupewa thawabu
kamilifu. 9 [h]Mtu yeyote asiyedumu katika
mafundisho ya Kristo, bali akayaacha,
yeye hana Mungu. Yeyote anayedumu
katika mafundisho ana Baba na Mwana
pia. 10 [i]Msimpokee mtu yeyote anayewajia
ambaye hawaletei mafundisho haya,
wala msimkaribishe nyumbani mwenu.
11 [j]Yeyote amkaribishaye mtu wa namna
hiyo anashiriki katika matendo maovu ya
mtu huyo.

*Salamu Za Mwisho*

12 [k]Ninayo mengi ya kuwaandikia, lakini
sitaki kutumia karatasi na wino. Badala
yake, nataraji kuja kwenu na kuongea
nanyi ana kwa ana, ili furaha yetu ipate
kuwa timilifu.
13 [l]Watoto wa dada yako mteule
wanakusalimu. Amen.

---

[a]**1:1** Mdo 11:30; 3Yn 1; Rum 16:13; 1Pet 5:13; Yn 8:32; 1Tim 2:4
[b]**1:2** 2Pet 1:12; Yn 14:17; 1Yn 1:8
[c]**1:3** Rum 1:7; 1Tim 1:2; 2Yn 1; 1:4; 3Yn 3, 4
[d]**1:5** 1Yn 2:7; 3:11
[e]**1:6** 1Yn 2:5; Yn 14:15; 1Yn 2:7
[f]**1:7** 1Yn 2:22; 4:2, 3; 4:1; 2:18
[g]**1:8** Mt 10:42; Ebr 11:26
[h]**1:9** 1Yn 2:23; Yn 8:31
[i]**1:10** Rum 16:17; 2The 3:6; 1Fal 13:17; 3Yn 8
[j]**1:11** 1Tim 5:22
[k]**1:12** 3Yn 13, 14; Yn 17:13; 1Yn 1:4
[l]**1:13** 1Pet 5:13; 2Yn 1

# 3 YOHANA

*Salamu*

[1] [a]Mzee:
Kwa Gayo rafiki yangu, nimpendaye
katika kweli.

*Gayo Anasifiwa Kwa Ajili Ya Ukarimu Wake*

[2] [b]Mpendwa, naomba ufanikiwe katika
mambo yote na kuwa na afya njema
kama vile roho yako ifanikiwavyo.
[3] [c]Ilinifurahisha sana baadhi ya ndugu
walipokuja na kutueleza juu ya uaminifu
wako katika kweli na jinsi unavyoendelea
kuenenda katika hiyo kweli. [4] [d]Sina furaha
kubwa kuliko hii, kusikia kwamba watoto
wangu wanaenenda katika kweli.
[5] [e]Rafiki mpendwa, wewe ni mwaminifu
kwa yale unayowatendea ndugu, ingawa
wao ni wageni kwako. [6] [f]Wameshuhudia
kuhusu upendo wako mbele ya kanisa.
Utafanya vyema ukiwasafirisha kama
inavyostahili kwa Mungu. [7] [g]Ilikuwa ni kwa
ajili ya hilo Jina waliondoka, bila kukubali
kupokea msaada wowote kutoka kwa watu
wasioamini. [8] [h]Kwa hiyo imetupasa sisi
kuonyesha ukarimu kwa watu kama hao
ili tuweze kutenda kazi pamoja kwa ajili
ya kweli.

*Deotrefe*

[9] Nililiandikia kanisa, lakini Deotrefe,
yeye apendaye kujifanya wa kwanza,
hakubali mamlaka yetu. [10] [i]Hivyo kama
nikija, nitakumbuka matendo yake
atendayo, akitusingizia kwa maneno ya hila.
Wala hatosheki na hayo anayotusingizia,
bali pia hukataa kuwakaribisha ndugu, na
hata huwazuia wale walio tayari kufanya
hivyo na kuwafukuza watoke kanisani.

*Demetrio*

[11] [j]Rafiki mpendwa, usiige lile lililo baya
bali lile lililo jema. Yeyote atendaye mema
atoka kwa Mungu, bali atendaye mabaya
hajamwona Mungu.
[12] [k]Kila mtu ameshuhudia mema kuhusu
Demetrio, vivyo hivyo hata na hiyo kweli
yenyewe. Sisi pia twashuhudia mema juu
yake, nanyi mwajua kwamba ushuhuda
wetu ni kweli.

*Salamu Za Mwisho*

[13] [l]Ninayo mambo mengi ya kukuandikia,
lakini sipendi kuandika kwa kalamu na
wino. [14] [m]Badala yake, nataraji kukuona
upesi, nasi tutaongea pamoja ana kwa ana.
[15] Amani iwe kwako. Rafiki zetu walioko
hapa wanakusalimu. Wasalimu hao rafiki
zetu walioko huko, kila mmoja kwa jina
lake.

---

[a]**1:1** Mdo 11:30; 2Yn 1
[b]**1:2** 2Yn 4
[c]**1:3** Mdo 1:16; 2Yn 4
[d]**1:4** 1Kor 4:14; 1Yn 1:2
[e]**1:5** Rum 12:13
[f]**1:6** 1Kor 16:11; 2Kor 1:16; Efe 4:1
[g]**1:7** Yn 15:21; Mdo 20:33, 35
[h]**1:8** Ebr 13:2; 2Yn 10
[i]**1:10** 3Yn 14; 2Yn 5; Yn 9:22, 34
[j]**1:11** Za 34:14; 37:27; 1Yn 2:29; 3:6, 9, 10
[k]**1:12** Yn 19:39; 21:24
[l]**1:13** 2Yn 12
[m]**1:14** 2Yn 12; Rum 1:7; Efe 6:23; Yn 10:3

# YUDA

### *Salamu*

1 [a]Yuda, mtumwa wa Yesu Kristo na
nduguye Yakobo:

Kwa wale walioitwa, wapendwa katika Mungu Baba na kuhifadhiwa salama ndani ya Yesu Kristo:

2 [b]Rehema, amani na upendo viwe kwenu
kwa wingi.

### *Dhambi Na Hukumu Ya Watu Wasiomcha Mungu*

3 [c]Wapendwa, ingawa nilikuwa
ninatamani sana kuwaandikia kuhusu
wokovu ambao tunaushiriki sisi sote,
niliona imenipasa kuwaandikia na kuwasihi
kwamba mwitetee imani iliyokabidhiwa
watakatifu kwa nafasi moja itoshayo. 4 [d]Kwa
kuwa kuna watu waliojipenyeza kwa siri
katikati yenu, watu walioandikiwa tangu
zamani hukumu hii, waovu, wapotoshao
neema ya Mungu wetu kuwa ufisadi
wakimkana yeye aliye Bwana wetu wa
pekee, Bwana Yesu Kristo.

### *Hukumu Kwa Walimu Wa Uongo*

5 [e]Ingawa mmekwisha kujua haya yote,
nataka niwakumbushe kuwa Bwana
akiisha kuwaokoa watu wake kutoka nchi
ya Misri, baadaye aliwaangamiza wale
ambao hawakuamini. 6 [f]Nao malaika ambao
hawakulinda nafasi zao, lakini wakayaacha
makao yao, hawa amewaweka katika giza,
wakiwa wamefungwa kwa minyororo ya
milele kwa ajili ya hukumu Siku ile kuu.
7 [g]Vivyo hivyo, Sodoma na Gomora na pia
ile miji iliyokuwa kandokando, ambayo
kwa jinsi moja na hao, walijifurahisha
kwa uasherati na kufuata tamaa za mwili
zisizo za asili, waliwekwa wawe mfano kwa
kuadhibiwa katika moto wa milele.
8 [h]Vivyo hivyo, hawa waotao ndoto
huutia mwili unajisi, hukataa kuwa chini
ya mamlaka na kunena mabaya juu ya
wenye mamlaka. 9 [i]Lakini hata malaika
mkuu Mikaeli alipokuwa anashindana na
ibilisi juu ya mwili wa Mose, hakuthubutu
kumlaumu, bali alimwambia, “Bwana na
akukemee!” 10 [j]Lakini watu hawa hunena
mabaya dhidi ya mambo wasiyoyafahamu.
Na katika mambo yale wanayoyafahamu
kwa hisia kama wanyama wasio na akili,
hayo ndiyo hasa yanayowaharibu.
11 [k]Ole wao! Kwa kuwa wanaifuata njia
ya Kaini, wamekimbilia faida katika kosa la
Balaamu na kuangamia katika uasi wa Kora.
12 [l]Watu hawa ni dosari katika karamu
zenu za upendo, wakila pamoja nanyi
bila hofu, wakijilisha pasipo hofu.
Wao ni mawingu yasiyokuwa na maji,
yakichukuliwa na upepo, miti isiyo na
matunda wakati wa mapukutiko, ambayo
hunyauka, iliyokufa mara mbili na
kung’olewa kabisa. 13 [m]Wao ni mawimbi
makali ya bahari, yakitoa povu la aibu yao
wenyewe, ni nyota zipoteazo, ambao weusi
wa giza ndio akiba waliowekewa milele.
14 [n]Enoki, mtu wa saba kuanzia Adamu
alitoa unabii kuhusu watu hawa, akisema:
“Tazama, Bwana anakuja pamoja na maelfu
kwa maelfu ya watakatifu wake, 15 [o]ili
kumhukumu kila mmoja na kuwapatiliza
wote wasiomcha Mungu kwa matendo
yao yote ya uasi waliyoyatenda, pamoja
na maneno yote ya kuchukiza ambayo

---

[a]**1:1** Yn 14:22; Mdo 1:13; Rum 1:6, 7; Yn 17:12
[b]**1:2** Rum 1:7; 2Pet 1:2
[c]**1:3** Tit 1:4; 1Tim 6:12
[d]**1:4** Gal 2:4; 2Pet 2:1; 1Yn 2:22
[e]**1:5** Kum 1:32; 1Kor 10:1-5
[f]**1:6** 2Pet 2:4, 9; Mwa 6:1; Yn 8:44; Ufu 20:10
[g]**1:7** Kum 29:23; Mt 25:41; Mwa 19:24; 2Pet 2:6, 10; Mt 10:15
[h]**1:8** 2Pet 2:10; Kut 22:28
[i]**1:9** Dan 12:1; Ufu 12:7; Zek 3:2
[j]**1:10** 2Pet 2:12
[k]**1:11** Mwa 4:3-8; 2Pet 2:15; Hes 16:1-3; 31:35
[l]**1:12** 2Pet 2:13; 1Kor 11:20-22; Mit 25:14; 2Pet 2:17; Efe 4:14; Mt 15:13
[m]**1:13** Isa 57:20; Flp 3:19; 2Pet 2:17
[n]**1:14** Mwa 5:18; 21:24; Kum 33:2; Dan 7:10
[o]**1:15** 2Pet 2:6-9; 1Tim 1:9

wenye dhambi wamesema dhidi yake.”
16 [a]Watu hawa ni wenye kunung’unika na
wenye kutafuta makosa; wao hufuata tamaa
zao mbaya, hujisifu kwa maneno makuu
kuhusu wao wenyewe na kuwasifu mno
watu wenye vyeo kwa ajili ya kujipatia
faida.

*Maonyo Na Mausia*

17 [b]Lakini ninyi wapenzi, kumbukeni yale
mitume wa Bwana Yesu Kristo waliyonena
zamani. 18 [c]Kwa kuwa waliwaambia, “Siku
za mwisho kutakuwa na watu wenye
kudhihaki, watakaofuata tamaa zao
wenyewe za upotovu.” 19 [d]Hawa ndio watu
wanaowagawa ninyi, wafuatao tamaa zao
za asili, wala hawana Roho.

20 [e]Lakini ninyi wapendwa, jijengeni
katika imani yenu iliyo takatifu sana tena
ombeni katika Roho Mtakatifu. 21 [f]Jilindeni
katika upendo wa Mungu mkitazamia kwa
furaha rehema ya Bwana wetu Yesu Kristo
ili awalete katika uzima wa milele.

22 Wahurumieni walio na mashaka;
23 [g]wengine waokoeni kwa kuwanyakua
kutoka kwenye moto; nao wengine
wahurumieni mkiwa na hofu, mkichukia
hata vazi lenye mawaa na kutiwa unajisi
na mwili.

*Dua Ya Kutakia Heri*

24 [h]Kwake yeye awezaye kuwalinda ninyi
msianguke na kuwaleta mbele za utukufu
wake mkuu bila dosari na kwa furaha
ipitayo kiasi: 25 [i]kwake yeye Mungu pekee
Mwokozi wetu, kwa Yesu Kristo Bwana
wetu, utukufu, ukuu, uweza na mamlaka
ni vyake tangu milele, sasa na hata milele!
Amen.

---

[a]**1:16** 2Pet 2:18; 2:10
[b]**1:17** 2Pet 3:2; Efe 4:11; Ebr 2:3
[c]**1:18** 1Tim 4:1; 2Pet 2:4
[d]**1:19** 1Kor 2:14, 15
[e]**1:20** Kol 2:7; Efe 6:18
[f]**1:21** Tit 2:13; 2Pet 3:12; Ebr 9:28; Mt 25:46
[g]**1:23** Amo 4:11; Zek 3:2-5; Ufu 3:4
[h]**1:24** Rum 16:25; 2Kor 4:14; Kol 1:22
[i]**1:25** Yn 5:44

# UFUNUO

*Utangulizi Na Salamu*

1 [a]Ufunuo wa Yesu Kristo aliopewa na
Mungu ili awaonyeshe watumishi wake
mambo ambayo ni lazima yatukie hivi
karibuni. Alijulisha mambo haya kwa
kumtuma malaika wake kwa Yohana
mtumishi wake, 2 [b]ambaye anashuhudia
kuhusu kila kitu alichokiona, yaani, Neno
la Mungu na ushuhuda wa Yesu Kristo.
3 [c]Amebarikiwa yeye asomaye maneno
ya unabii huu, na wamebarikiwa wale
wanaoyasikia na kuyatia moyoni yale
yaliyoandikwa humo, kwa sababu wakati
umekaribia.

*Salamu Kwa Makanisa Saba*

4 [d]Yohana, kwa makanisa saba yaliyoko
Asia:

Neema na amani iwe kwenu kutoka
kwake aliyeko, aliyekuwako na atakayekuja,
na kutoka kwa wale roho saba walioko
mbele ya kiti chake cha enzi, 5 [e]na kutoka
kwa Yesu Kristo ambaye ni yule shahidi
mwaminifu, mzaliwa wa kwanza kutoka
kwa wafu, mtawala wa wafalme wa dunia.

Kwake yeye anayetupenda na ambaye
ametuweka huru kutoka dhambi zetu kwa
damu yake, 6 [f]akatufanya sisi kuwa ufalme
na makuhani, tumtumikie Mungu wake
ambaye ni Baba yake. Utukufu na uwezo
ni vyake milele na milele! Amen.

7 [g]Tazama! Anakuja na mawingu,
na kila jicho litamwona,
hata wale waliomchoma;
na makabila yote duniani
yataomboleza kwa sababu yake.
Naam, ndivyo itakavyokuwa! Amen.

8 [h]“Mimi ni Alfa na Omega,” asema
Bwana Mungu, “aliyeko, aliyekuwako na
atakayekuja, Mwenyezi.”

*Maono Ya Kristo*

9 [i]Mimi, Yohana, ndugu yenu ninayeshiriki
pamoja nanyi mateso katika Yesu na katika
ufalme na uvumilivu katika saburi, nilikuwa
katika kisiwa cha Patmo kwa ajili ya neno
la Mungu na ushuhuda wa Yesu. 10 [j]Katika
siku ya Bwana, nilikuwa katika Roho na
nikasikia sauti kubwa kama ya baragumu
nyuma yangu 11 [k]ikisema, “Andika kwenye
kitabu haya yote unayoyaona, kisha
uyapeleke kwa makanisa saba, yaani: Efeso,
Smirna, Pergamo, Thiatira, Sardi, Filadelfia
na Laodikia.”

12 [l]Ndipo nikageuka ili nione ni sauti
ya nani iliyokuwa ikisema nami. Nami
nilipogeuka, nikaona vinara saba vya taa
vya dhahabu, 13 [m]na katikati ya vile vinara
vya taa, alikuwamo mtu kama Mwana
wa Adamu, akiwa amevaa joho refu, na
mkanda wa dhahabu ukiwa umefungwa
kifuani mwake. 14 [n]Kichwa chake na nywele
zake zilikuwa nyeupe kama sufu, nyeupe
kama theluji, nayo macho yake yalikuwa
kama mwali wa moto. 15 [o]Nyayo zake
zilikuwa kama shaba inayong’aa, katika
tanuru ya moto, nayo sauti yake ilikuwa
kama mugurumo ya maji mengi. 16 [p]Katika
mkono wake wa kuume alishika nyota saba,
na kinywani mwake ulitoka upanga mkali

[a]**1:1** Ufu 22:16; Dan 2:28, 29; Yn 12:49; 17:8, 19; Ufu 22:6
[b]**1:2** 1Kor 1:6; Ufu 6:9; Ebr 4:12; Ufu 12:17; 19:10
[c]**1:3** Lk 11:28; Ufu 22:7; Rum 13:11
[d]**1:4** Isa 11:2; Rum 1:7; Ufu 4:8; 11:17; 3:1; 4:5; 5:6
[e]**1:5** Isa 55:4; Kol 1:18; Ufu 17:14
[f]**1:6** 1Pet 2:5; Rum 11:36
[g]**1:7** Dan 7:13; Zek 12:10
[h]**1:8** Ufu 22:6; 4:8; 21:6; 22:13; 15:3; Kut 3:14; Isa 41:4; Ufu 21:6
[i]**1:9** Mdo 14:22; 2Tim 2:12
[j]**1:10** Ufu 17:3; 3:1
[k]**1:11** Ufu 2:8; 22:13; Mdo 18:19; Kol 2:1; Mdo 16:14
[l]**1:12** Zek 1:2; Ufu 3:1
[m]**1:13** Eze 1:26; Ufu 14:14; Dan 10:5; Ufu 15:6
[n]**1:14** Dan 7:9; Ufu 19:12
[o]**1:15** Eze 1:7; 43:2; Ufu 2:18; 19:6
[p]**1:16** Ufu 3:1; Isa 1:20; Ebr 4:12

wenye makali kuwili. Uso wake ulikuwa
kama jua liking'aa kwa nguvu zake zote.
17 [a]Nilipomwona, nilianguka miguuni
pake kama aliyekufa. Ndipo akauweka
mkono wake wa kuume juu yangu na
kusema: "Usiogope, Mimi ndiye wa Kwanza
na wa Mwisho. 18 [b]Mimi ni Yeye Aliye Hai,
niliyekuwa nimekufa, na tazama, ni hai
milele na milele! Nami ninazo funguo za
mauti na kuzimu.[c]
19 [d]"Basi andika mambo uliyoyaona,
yaliyopo na yale yatakayotukia baada ya
haya. 20 [e]Kuhusu siri ya zile nyota saba
ulizoziona katika mkono wangu wa kuume
na vile vinara saba vya taa vya dhahabu
ni hii: Zile nyota saba ni malaika wa yale
makanisa saba, navyo vile vinara saba ni
hayo makanisa saba.

*Kwa Kanisa Lililoko Efeso*

2 [f]"Kwa malaika wa kanisa lililoko Efeso
andika:

"Haya ndiyo maneno ya yule
aliyezishika zile nyota saba katika
mkono wake wa kuume na ambaye
hutembea kati ya vile vinara saba vya
taa vya dhahabu. 2 [g]Nayajua matendo
yako, bidii yako na saburi yako. Najua
kuwa huwezi kuvumiliana na watu
waovu na ya kwamba umewajaribu
wale wanaojifanya kuwa mitume
na kumbe sio, nawe umewatambua
kuwa ni waongo. 3 [h]Umevumilia na
kustahimili taabu kwa ajili ya Jina
langu, wala hukuchoka.
4 [i]"Lakini nina neno dhidi yako:
Umeuacha upendo wako wa kwanza.
5 [j]Kumbuka basi ni wapi ulikoangukia!
Tubu na ukafanye matendo yale ya
kwanza. Kama usipotubu, nitakuja
kwako na kukiondoa kinara chako
cha taa kutoka mahali pake. 6 [k]Lakini
una jambo hili kwa upande wako:
Unayachukia matendo ya Wanikolai,
ambayo nami pia nayachukia.
7 [l]"Yeye aliye na sikio na asikie yale
ambayo Roho ayaambia makanisa.
Yeye ashindaye, nitampa haki ya
kula matunda toka kwa mti wa uzima,
ambao uko katika paradiso[m] ya Mungu.

*Kwa Kanisa Lililoko Smirna*

8 [n]"Kwa malaika wa kanisa lililoko Smirna
andika:

"Haya ndiyo maneno yake yeye aliye
wa Kwanza na wa Mwisho, aliyekufa
kisha akafufuka. 9 [o]Naijua dhiki yako na
umaskini wako, lakini wewe ni tajiri!
Nayajua masingizio ya wale wasemao
kuwa ni Wayahudi lakini sio, bali wao
ni sinagogi la Shetani. 10 [p]Usiogope
mateso yatakayokupata. Nakuambia
ibilisi atawatia baadhi yenu gerezani ili
kuwajaribu, nanyi mtapata dhiki kwa
muda wa siku kumi. Uwe mwaminifu
hata kufa, nami nitakupa taji ya uzima.
11 [q]"Yeye aliye na sikio na asikie yale
ambayo Roho ayaambia makanisa.
Yeye ashindaye hatadhuriwa kamwe
na mauti ya pili.

*Kwa Kanisa Lililoko Pergamo*

12 [r]"Kwa malaika wa Kanisa lililoko
Pergamo andika:

"Haya ndiyo maneno yake yeye

---

[a]**1:17** Eze 1:28; Dan 8:17, 18; Isa 48:12; Ufu 22:13
[b]**1:18** Rum 6:9; Kum 32:40; Ufu 9:1
[c]18 Kuzimu linalotokana na neno Hades la Kiyunani au Sheol kwa Kiebrania; maana yake ni mahali pa mateso kwa watu waliopotea.
[d]**1:19** Ufu 1:11; Hab 2:2
[e]**1:20** Zek 4:2; Mt 5:14, 15
[f]**2:1** Ufu 1:16; 1:12-13
[g]**2:2** 1Yn 4:1; 2Kor 11:13
[h]**2:3** Yn 15:21
[i]**2:4** Yer 2:2; Mt 24:12
[j]**2:5** Ufu 1:20
[k]**2:6** Ufu 2:15; Za 139:21
[l]**2:7** Mt 11:15; Ufu 13:9; Mwa 2:9; Ufu 22:2, 14; Lk 23:43
[m]7 Paradiso hapa ina maana ya Bustani, yaani shamba dogo la miti izaayo matunda.
[n]**2:8** Ufu 1:11-13
[o]**2:9** Yak 2:5; Ufu 3:9; Mt 4:10
[p]**2:10** Ufu 3:10; Dan 1:12-14
[q]**2:11** Ufu 20:6-14; 21:8
[r]**2:12** Ufu 1:11-16; 1:17, 18; 2:7

aliye na upanga mkali wenye makali
kuwili. 13 [a]Ninajua unakoishi, ni kule
ambako Shetani ana kiti chake cha
enzi. Lakini umelishika Jina langu.
Wala hukuikana imani yako kwangu
hata katika siku za shahidi wangu
mwaminifu Antipa, ambaye aliuawa
katika mji mkuu wenu, ambako ndiko
anakoishi Shetani.

14 [b]"Hata hivyo, nina mambo
machache dhidi yako: Unao watu
wafuatao mafundisho ya Balaamu, yule
aliyemfundisha Balaki kuwashawishi
Waisraeli watende dhambi kwa kula
vitu vilivyotolewa kafara kwa sanamu
na kufanya uasherati. 15 [c]Vivyo hivyo
unao wale wayashikayo mafundisho
ya Wanikolai. 16 [d]Basi tubu! Ama sivyo,
nitakuja kwako upesi na kupigana
na watu hao kwa upanga wa kinywa
changu.

17 [e]"Yeye aliye na sikio na asikie yale
ambayo Roho ayaambia makanisa.
Yeye ashindaye nitampa baadhi ya ile
mana iliyofichwa. Nitampa pia jiwe
jeupe ambalo juu yake limeandikwa
jina jipya asilolijua mtu, isipokuwa
yule anayelipokea.

### *Kwa Kanisa Lililoko Thiatira*

18 [f]"Kwa malaika wa kanisa lililoko
Thiatira andika:

"Haya ndiyo maneno ya Mwana wa
Mungu, ambaye macho yake ni kama
mwali wa moto na ambaye miguu yake
ni kama shaba iliyosuguliwa sana.
19 [g]Nayajua matendo yako, upendo
wako na imani yako, huduma na saburi
yako na kwamba matendo yako ya sasa
yamezidi yale ya kwanza.

20 [h]"Hata hivyo, nina neno dhidi
yako: Unamvumilia yule mwanamke
Yezebeli ambaye anajiita nabii, lakini
anawafundisha na kuwapotosha
watumishi wangu ili wafanye uasherati
na kula vyakula vilivyotolewa kafara
kwa sanamu. 21 [i]Nimempa muda ili
atubu kwa ajili ya uasherati wake,
lakini hataki. 22 [j]Kwa hiyo nitamtupa
kwenye kitanda cha mateso, na
nitawafanya hao wanaozini naye
kupata mateso makali wasipotubia njia
zake. 23 [k]Nami nitawaua watoto wake.
Nayo makanisa yote yatajua kwamba
Mimi ndiye nichunguzaye mioyo
na nia, na kwamba nitamlipa kila
mmoja wenu kwa kadiri ya matendo
yake. 24 [l]Basi nawaambia ninyi
wengine mlioko Thiatira, ninyi ambao
hamyafuati mafundisho ya Yezebeli,
wala hamkujifunza hayo yanayoitwa
mambo ya ndani sana ya Shetani
(sitaweka mzigo mwingine wowote juu
yenu): 25 [m]Lakini shikeni sana mlicho
nacho, mpaka nitakapokuja.

26 [n]"Atakayeshinda na kutenda
mapenzi yangu mpaka mwisho,
nitampa mamlaka juu ya mataifa:

27 [o]" 'Atawatawala kwa fimbo ya
chuma,
atawavunja vipande vipande
kama chombo cha udongo':

kama vile mimi nilivyopokea mamlaka
kutoka kwa Baba yangu. 28 [p]Nami
nitampa pia ile nyota ya asubuhi.
29 Yeye aliye na sikio na asikie yale
ambayo Roho ayaambia makanisa.

### *Kwa Kanisa Lililoko Sardi*

3 [q]"Kwa malaika wa kanisa lililoko Sardi
andika:

"Haya ndiyo maneno ya aliye na

[a]**2:13** Ufu 14:12
[b]**2:14** 1Pet 2:15; 1Kor 6:13
[c]**2:15** Ufu 2:6
[d]**2:16** 2The 2:8
[e]**2:17** Yn 6:49-50; Isa 62:2; Ufu 19:12
[f]**2:18** Ufu 1:11-15
[g]**2:19** Ufu 2:2
[h]**2:20** 1Fal 21:25; 2Fal 9:7
[i]**2:21** Rum 2:4; Ufu 9:20
[j]**2:22** Ufu 17:2; 18:9
[k]**2:23** 1Sam 16:7; Yer 11:20
[l]**2:24** Mdo 15:28
[m]**2:25** Ufu 3:11
[n]**2:26** Za 2:8; Ufu 3:21
[o]**2:27** Ufu 12:5; Za 2:9; Yer 19:11
[p]**2:28** Ufu 22:16
[q]**3:1** Ufu 1:4; 1:16; 2:2; 1Tim 5:6

zile Roho saba[a] za Mungu na zile nyota saba. Nayajua matendo yako, kwamba una sifa ya kuwa hai, lakini umekufa. 2 [b]Amka! Nawe uyaimarishe yale yaliyosalia na yaliyo karibu kufa, kwa maana sikuona kwamba kazi zako zimekamilika machoni pa Mungu wangu. 3 [c]Kumbuka basi yale uliyoyapokea na kuyasikia, yatii na ukatubu. Lakini usipoamka, nitakuja kama mwizi wala hutajua saa nitakayokuja kwako.

4 [d]"Lakini bado una watu wachache katika Sardi ambao hawajayachafua mavazi yao. Wao wataenda pamoja nami, wakiwa wamevaa mavazi meupe, kwa maana wanastahili. 5 [e]Yeye ashindaye atavikwa vazi jeupe kama wao. Sitafuta jina lake kutoka kitabu cha uzima, bali nitalikiri jina lake mbele za Baba yangu na mbele za malaika wake. 6 [f]Yeye aliye na sikio na asikie yale ambayo Roho ayaambia makanisa.

*Kwa Kanisa Lililoko Filadelfia*

7 [g]"Kwa malaika wa kanisa lililoko Filadelfia andika:

"Haya ndiyo maneno yake yeye aliye mtakatifu na wa kweli, yeye aliye na ufunguo wa Daudi. Anachokifungua hakuna awezaye kukifunga, wala anachokifunga hakuna awezaye kukifungua. 8 [h]Nayajua matendo yako. Tazama, nimeweka mbele yako mlango uliofunguliwa, wala hakuna awezaye kuufunga. Ninajua kwamba una nguvu kidogo lakini umelishika neno langu wala hukulikana Jina langu. 9 [i]Nitawafanya wale wa sinagogi la Shetani, wale ambao husema kuwa ni Wayahudi lakini sio, bali ni waongo, nitawafanya waje wapige magoti miguuni pako, na wakiri ya kwamba nimekupenda. 10 [j]Kwa kuwa umeshika amri yangu ya kuvumilia katika saburi, nitakulinda katika saa ya kujaribiwa inayokuja ulimwenguni pote, ili kuwajaribu wote wakaao duniani.

11 [k]"Ninakuja upesi. Shika sana ulicho nacho, ili mtu asije akaichukua taji yako. 12 [l]Yeye ashindaye nitamfanya kuwa nguzo katika hekalu la Mungu wangu, wala hatatoka humo kamwe. Nitaandika juu yake Jina la Mungu wangu na jina la mji mkubwa wa Mungu wangu, Yerusalemu mpya, ambao unashuka kutoka mbinguni kwa Mungu wangu. Nami pia nitaandika juu yake Jina langu jipya. 13 [m]Yeye aliye na sikio na asikie yale ambayo Roho ayaambia makanisa.

*Kwa Kanisa Lililoko Laodikia*

14 [n]"Kwa malaika wa kanisa lililoko Laodikia andika:

"Haya ndiyo maneno yake yeye aliye Amen, shahidi mwaminifu na wa kweli, mtawala wa uumbaji wote wa Mungu. 15 [o]Nayajua matendo yako, ya kwamba wewe si baridi wala si moto. Afadhali ungelikuwa moja au lingine. 16 Hivyo kwa kuwa u vuguvugu, si baridi wala moto, nitakutapika utoke kinywani mwangu. 17 [p]Kwa maana unasema: 'Mimi ni tajiri, nimejilimbikizia mali, wala sihitaji kitu chochote.' Lakini hutambui ya kwamba wewe ni mnyonge, wa kuhurumiwa, maskini, kipofu, tena uliye uchi. 18 [q]Nakushauri

---

[a]1 Roho saba za Mungu hapa inamaanisha Roho wa Mungu katika ukamilifu wa utendaji wake.
[b]**3:2** Eze 34:4
[c]**3:3** Ufu 2:5; 2Pet 3:10
[d]**3:4** Yud 23; Ufu 6:11
[e]**3:5** Ufu 20:12; Mt 10:32
[f]**3:6** Ufu 2:7
[g]**3:7** Yn 5:20; Isa 22:22; Mt 16:19
[h]**3:8** Mdo 14:27; Ufu 2:13
[i]**3:9** Ufu 2:9; Isa 49:23; 43:4
[j]**3:10** 2Pet 2:9; Ufu 2:10; 11:10; 17:8
[k]**3:11** Ufu 2:25; Mt 16:27; Ufu 2:25; 1Kor 9:25
[l]**3:12** Gal 2:9; Ufu 14:1; 22:4; 21:2-10
[m]**3:13** Ufu 2:7
[n]**3:14** Kol 1:16-18
[o]**3:15** Rum 12:11
[p]**3:17** Hos 12:8; 1Kor 4:8
[q]**3:18** Ufu 16:15

ununue kutoka kwangu dhahabu
iliyosafishwa kwa moto, ili upate kuwa
tajiri, na mavazi meupe ili uyavae
upate kuficha aibu ya uchi wako, na
mafuta ya kupaka macho yako ili upate
kuona.
19 [a]"Wale niwapendao, ninawakemea
na kuwaadibisha. Hivyo uwe na bidii
ukatubu. 20 [b]Tazama! Nasimama
mlangoni nabisha. Kama mtu yeyote
akisikia sauti yangu na kufungua
mlango, nitaingia ndani na kula
pamoja naye, naye pamoja nami.
21 [c]"Yeye ashindaye nitampa haki
ya kuketi pamoja nami kwenye kiti
changu cha enzi, kama vile mimi
nilivyoshinda na nikaketi pamoja na
Baba yangu kwenye kiti chake cha enzi.
22 [d]Yeye aliye na sikio na asikie yale
ambayo Roho ayaambia makanisa."

### *Kiti Cha Enzi Kilichoko Mbinguni*

4 [e]Baada ya mambo hayo nilitazama, nami
nikaona mbele yangu mlango uliokuwa
wazi mbinguni. Nayo ile sauti niliyokuwa
nimeisikia hapo mwanzo ikisema nami
kama tarumbeta ikasema, "Njoo, huku,
nami nitakuonyesha yale ambayo hayana
budi kutokea baada ya haya." 2 [f]Ghafula
nilikuwa katika Roho, na hapo mbele
yangu kilikuwepo kiti cha enzi mbinguni,
kikiwa kimekaliwa na mtu. 3 [g]Aliyekuwa
amekikalia alikuwa anaonekana kama yaspi
na akiki. Kukizunguka kile kiti cha enzi
palikuwa na upinde wa mvua ulioonekana
kama zumaridi.
4 [h]Kukizunguka hicho kiti cha enzi
palikuwa na viti vingine vya enzi ishirini
na vinne, na juu ya hivyo viti walikuwa
wameketi wazee ishirini na wanne. Walivaa
mavazi meupe, na walikuwa na taji za
dhahabu vichwani mwao. 5 [i]Kwenye kile
kiti cha enzi palikuwa panatoka miali ya
umeme wa radi, ngurumo na sauti za radi.
Mbele ya kiti cha enzi, taa saba zilikuwa
zinawaka. Hizi ndizo roho saba[j] za Mungu.
6 [k]Pia mbele ya kiti cha enzi palikuwa na
kile kilichoonekana kama bahari ya kioo,
iliyokuwa angavu kama bilauri.
Katikati, kukizunguka kile kiti cha enzi,
kulikuwa na viumbe wanne wenye uhai,
wakiwa wamejawa na macho mbele na
nyuma. 7 [l]Kiumbe wa kwanza mwenye
uhai alikuwa kama simba, wa pili alikuwa
kama ng'ombe dume, wa tatu alikuwa
na uso kama wa mwanadamu, na wa
nne alikuwa kama tai anayeruka. 8 [m]Kila
mmoja wa hawa viumbe wanne wenye
uhai alikuwa na mabawa sita, na kujawa
na macho pande zote hadi chini ya mabawa.
Usiku na mchana hawaachi kusema:

"Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu,
ni BWANA Mungu Mwenyezi,
aliyekuwako, aliyeko na atakayekuja."

9 [n]Kila mara viumbe hao wanne wenye
uhai wanapomtukuza, kumheshimu na
kumshukuru yeye aketiye kwenye kile kiti
cha enzi, tena aishiye milele na milele,
10 [o]wale wazee ishirini na wanne huanguka
mbele zake aketiye kwenye kiti cha enzi
na kumwabudu yeye aliye hai milele na
milele. Huziweka taji zao mbele ya kiti cha
enzi, wakisema:

11 [p]"Bwana wetu na Mungu wetu,
wewe unastahili kupokea utukufu
na heshima na uweza,
kwa maana ndiwe uliyeviumba vitu
vyote,
na kwa mapenzi yako viliumbwa
na vimekuwako."

---

[a]**3:19** Kum 8:5; 1Kor 11:32; Ufu 2:5
[b]**3:20** Mt 24:33; Lk 12:36; Yn 14:23
[c]**3:21** Mt 19:28; Ufu 5:5
[d]**3:22** Ufu 2:7
[e]**4:1** Ufu 1:10; 11:12; 1:19
[f]**4:2** 1Fal 22:19; Ufu 20:11
[g]**4:3** Eze 1:28
[h]**4:4** Ufu 11:16; 3:4-5
[i]**4:5** Kut 19:16; Zek 4:2; Ufu 1:4
[j]5 Roho saba za Mungu hapa inamaanisha Roho wa Mungu katika ukamilifu wa utendaji wake.
[k]**4:6** Ufu 15:2; Eze 1:5-10
[l]**4:7** Eze 10:14
[m]**4:8** Isa 6:2-3; Ufu 1:4-8
[n]**4:9** Za 47:8
[o]**4:10** Kum 33:3
[p]**4:11** Ufu 1:6; 10:6

*Kitabu Na Mwana-Kondoo*

5 [a]Kisha nikaona katika mkono wake wa
kuume wa yule aliyeketi kwenye kile
kiti cha enzi, kitabu kilichoandikwa ndani
na upande wa nje, kikiwa kimefungwa
kwa lakiri saba. 2 [b]Nami nikamwona
malaika mwenye nguvu akitangaza kwa
sauti kuu, akisema, “Ni nani anayestahili
kuzivunja hizo lakiri na kukifungua
kitabu?” 3 [c]Lakini hapakuwa na yeyote
mbinguni wala duniani au chini ya dunia
aliyeweza kukifungua hicho kitabu wala
hata kutazama ndani yake. 4 Nikalia sana
sana kwa sababu hakuonekana yeyote
anayestahili kukifungua hicho kitabu wala
kutazama ndani yake. 5 [d]Kisha, mmoja wa
wale wazee akaniambia, “Usilie! Tazama,
Simba wa kabila la Yuda, wa Uzao wa
Daudi, ameshinda. Yeye ndiye anayeweza
kukifungua hicho kitabu na kuvunja hizo
lakiri zake saba.”

6 [e]Ndipo nikaona katikati ya kile kiti cha
enzi na wale viumbe wenye uhai wanne na
miongoni mwa wale wazee, Mwana-Kondoo
amesimama, akiwa kama amechinjwa.
Alikuwa na pembe saba na macho saba,
ambazo ndizo zile Roho saba[f] za Mungu
zilizotumwa duniani pote. 7 [g]Huyo Mwana-
Kondoo akaja na kukitwaa kile kitabu
kutoka kwenye mkono wa kuume wa
yule aliyeketi kwenye kile kiti cha enzi.
8 [h]Alipokwisha kukitwaa kile kitabu, wale
viumbe wenye uhai wanne pamoja na
wale wazee ishirini na wanne wakaanguka
mbele ya yule Mwana-Kondoo. Kila mmoja
wao alikuwa na kinubi, nao walikuwa
wameshika mabakuli ya dhahabu yaliyojaa
uvumba, ambayo ni maombi ya watakatifu.
9 [i]Nao wakaimba wimbo mpya, wakisema:

“Wewe unastahili kukitwaa kitabu
na kuzivunja lakiri zake,
kwa sababu ulichinjwa
na kwa damu yako ukamnunulia
Mungu watu
kutoka kila kabila, kila lugha,
kila jamaa na kila taifa.
10 [j]Wewe umewafanya hawa wawe
ufalme na makuhani
wa kumtumikia Mungu wetu,
nao watatawala duniani.”

11 [k]Kisha nikatazama, nikasikia sauti za
malaika wengi wakiwa wamekizunguka
kile kiti cha enzi, pamoja na wale viumbe
wenye uhai wanne na wale wazee ishirini
na wanne. Idadi yao ilikuwa kumi elfu mara
kumi elfu na maelfu ya maelfu. 12 [l]Nao
waliimba kwa sauti kuu, wakisema:

“Anastahili Mwana-Kondoo, yeye
aliyechinjwa,
kupokea uweza na utajiri na
hekima na nguvu
na heshima na utukufu na sifa!”

13 [m]Kisha nikasikia kila kiumbe mbinguni
na duniani, chini ya nchi na baharini na
vyote vilivyomo ndani yake vikiimba:

“Sifa na heshima na utukufu na
uweza
ni vyake yeye aketiye juu ya hicho
kiti cha enzi
na kwa Mwana-Kondoo,
milele na milele!”

14 [n]Wale viumbe wenye uhai wanne
wakasema, “Amen!” Nao wale wazee
ishirini na wanne wakaanguka kifudifudi
wakaabudu.

---

[a]**5:1** Ufu 4:2, 9; Eze 2:9-10; Isa 29:11; Dan 12:4
[b]**5:2** Ufu 10:1
[c]**5:3** Ufu 5:13
[d]**5:5** Mwa 49:9; Isa 11:1, 10; Rum 15:12
[e]**5:6** Yn 1:29; Zek 4:10
[f]6 Roho saba za Mungu hapa inamaanisha Roho wa Mungu katika ukamilifu wa utendaji wake.
[g]**5:7** Ufu 4:2
[h]**5:8** Ufu 14:2; Za 141:2
[i]**5:9** Za 149:1; Ufu 14:3-4; 4:11; Ebr 9:12; 1Kor 6:20
[j]**5:10** 1Pet 5:5
[k]**5:11** Dan 7:10; Yud 14
[l]**5:12** Ufu 4:11
[m]**5:13** Flp 2:10; Mal 1:6; Rum 11:36
[n]**5:14** Ufu 4:9-10; 19:4

*Mwana-Kondoo Avunja Lakiri Saba*

6 [a]Kisha nikaangalia wakati Mwana-
Kondoo akivunja ile lakiri ya kwanza
miongoni mwa zile saba. Ndipo nikasikia
mmoja wa wale viumbe wanne wenye
uhai akisema kwa sauti kama ya radi:
"Njoo!" 2 [b]Nikatazama, na hapo mbele
yangu alikuwepo farasi mweupe! Yeye
aliyempanda alikuwa na upinde, naye
akapewa taji, akampanda akatoka akiwa
kama mshindi aelekeaye katika kushinda.
3 [c]Alipoivunja ile lakiri ya pili, nikamsikia
yule kiumbe wa pili mwenye uhai akisema,
"Njoo!" 4 [d]Ndipo akatokea farasi mwingine
mwekundu sana. Yeye aliyempanda
akapewa uwezo wa kuondoa amani duniani
na kuwafanya watu wauane. Yeye akapewa
upanga mkubwa.
5 [e]Mwana-kondoo alipoivunja ile lakiri
ya tatu, nikamsikia yule kiumbe wa tatu
mwenye uhai akisema, "Njoo!" Nikatazama,
na mbele yangu alikuwepo farasi mweusi!
Yeye aliyempanda alikuwa na mizani
mkononi mwake. 6 [f]Ndipo nikasikia kile
kilichokuwa kama sauti katikati ya wale
viumbe wanne wenye uhai ikisema,
"Kipimo kimoja[g] cha ngano kwa mshahara
wa kibarua wa siku moja,[h] na vipimo vitatu
vya shayiri kwa mshahara wa kibarua cha
siku moja. Lakini usiharibu mafuta wala
divai!"
7 [i]Alipovunja ile lakiri ya nne, nikasikia
sauti ya yule kiumbe wa nne mwenye uhai
ikisema, "Njoo!" 8 [j]Nikatazama, na hapo
mbele yangu alikuwepo farasi mwenye rangi
ya kijivujivu! Yeye aliyempanda aliitwa
Mauti, naye Kuzimu[k] alikuwa akimfuata
nyuma yake kwa karibu. Wakapewa
mamlaka juu ya robo ya dunia, kuua kwa
upanga, njaa, tauni na kwa wanyama
wakali wa dunia.
9 [l]Mwana-kondoo alipoivunja ile lakiri
ya tano, nikaona chini ya madhabahu,
roho za wale waliochinjwa kwa ajili ya
neno la Mungu na kwa ajili ya ushuhuda
walioutunza. 10 [m]Wakalia kwa sauti
kuu, wakisema, "Hata lini, Ee Bwana
Mwenyezi, uliye mtakatifu na mwaminifu,
hutawahukumu na kulipiza kisasi juu ya
watu waishio duniani kwa ajili ya damu
yetu?" 11 [n]Kisha kila mmoja wao akapewa
joho jeupe na wakaambiwa wangoje kwa
muda kidogo zaidi, mpaka idadi ya ndugu
zao na watumishi wenzao watakaouawa
kama wao walivyouawa, itakapotimia.
12 [o]Nikatazama akiivunja ile lakiri ya
sita. Pakatokea tetemeko kuu la nchi,
na jua likawa jeusi kama nguo ya gunia
iliyotengenezwa kwa singa za mbuzi, na
mwezi wote ukawa mwekundu kama damu.
13 [p]Nyota zilizo angani zikaanguka ardhini
kama vile matunda ya mtini yasiyokomaa
yaangukavyo wakati mti wake unapotikiswa
na upepo mkali. 14 [q]Anga ikatoweka kama
vile karatasi isokotwavyo, na kila mlima
na kila kisiwa kikaondolewa mahali pake.
15 [r]Ndipo wafalme wa dunia, wakuu wote,
majemadari, matajiri, wenye nguvu na kila
mtu, mtumwa na mtu huru, wakajificha
katika mapango na kwenye miamba ya
milima. 16 [s]Wakaiita milima na miamba
wakisema, "Tuangukieni, mkatufiche na
uso wake yeye aketiye kwenye kiti cha
enzi, na mkatuepushe na ghadhabu ya
Mwana-Kondoo! 17 [t]Kwa maana siku ile
kuu ya ghadhabu yao imewadia. Je, ni nani
awezaye kustahimili?"

[a]**6:1** Ufu 5:6; 5:1; 19:6; 4:6-7; 14:2
[b]**6:2** Zek 1:8; 6:11; Ufu 19:11-12; Za 45:4
[c]**6:3** Ufu 4:7
[d]**6:4** Zek 1:8; 6:2; Mt 10:34
[e]**6:5** Ufu 4:7
[f]**6:6** Ufu 4:6-7; 7:1-3
[g]6 Ni kama lita moja.
[h]6 Sawa na dinari moja.
[i]**6:7** Zek 6:3; Hos 13:14; Yer 24:10; Eze 5:12-17
[j]**6:8** Zek 6:3; Hos 13:14; Ufu 1:18; 20:13; 14; Yer 15:2, 3; 24:10; Eze 5:12, 17
[k]8 Kuzimu linalotokana na neno Hades la Kiyunani au Sheol kwa Kiebrania.
[l]**6:9** Ufu 14:18; 16:17; 20:4
[m]**6:10** Za 119:84; 79:10; Zek 1:12; Ufu 3:7; 18:20
[n]**6:11** Ufu 3:4; Ebr 11:40
[o]**6:12** Isa 29:6; Ufu 16:18; Mt 24:29
[p]**6:13** Ufu 9:1; Isa 34:4
[q]**6:14** Isa 54:10; Ufu 21:1
[r]**6:15** Isa 2:10-21
[s]**6:16** Hos 10:8; Lk 23:30
[t]**6:17** Yoe 1:15; Ufu 16:14; Nah 1:6; Mal 3:2

*Waisraeli 144,000 Watiwa Muhuri*

7 [a]Baada ya hili nikaona malaika wanne
wakiwa wamesimama katika pembe
nne za dunia, wakizuia hizo pepo nne
za dunia, ili kwamba pasiwe na upepo
utakaovuma juu ya nchi au juu ya bahari
au juu ya mti wowote. 2 [b]Nikaona malaika
mwingine akipanda kutoka mawio ya jua
akiwa na muhuri wa Mungu aliye hai.
Akawaita kwa sauti kubwa wale malaika
wanne waliokuwa wamepewa mamlaka
ya kuidhuru nchi na bahari, akisema,
3 [c]"Msiidhuru nchi wala bahari, wala miti,
hadi tuwe tumetia muhuri kwenye vipaji
vya nyuso za watumishi wa Mungu wetu."
4 [d]Ndipo nikasikia idadi ya wale waliotiwa
muhuri: yaani 144,000 kutoka makabila
yote ya Israeli.

5 Kutoka kabila la Yuda 12,000
walitiwa muhuri,
kutoka kabila la Reubeni 12,000,
kutoka kabila la Gadi 12,000,
6 kutoka kabila la Asheri 12,000,
kutoka kabila la Naftali 12,000,
kutoka kabila la Manase 12,000,
7 kutoka kabila la Simeoni 12,000,
kutoka kabila la Lawi 12,000,
kutoka kabila la Isakari 12,000,
8 kutoka kabila la Zabuloni 12,000,
kutoka kabila la Yosefu 12,000,
na kutoka kabila la Benyamini
12,000.

*Umati Mkubwa Wa Watu Kutoka Mataifa Yote*

9 [e]Baada ya hili nikatazama na hapo mbele
yangu palikuwa na umati mkubwa wa watu
ambao hakuna yeyote awezaye kuuhesabu,
kutoka kila taifa, kila kabila, kila jamaa
na kila lugha, wamesimama mbele ya kile
kiti cha enzi na mbele ya Mwana-Kondoo.
Walikuwa wamevaa mavazi meupe na
wakiwa wameshika matawi ya mitende
mikononi mwao. 10 [f]Nao walikuwa wakipiga
kelele kwa sauti kubwa wakisema:

"Wokovu una Mungu wetu,
yeye aketiye kwenye kiti cha enzi,
na Mwana-Kondoo!"

11 [g]Malaika wote walikuwa wamesimama
kukizunguka kile kiti cha enzi na wale
wazee ishirini na wanne na wale viumbe
wanne wenye uhai. Wakaanguka kifudifudi
mbele ya hicho kiti cha enzi na kumwabudu
Mungu, 12 [h]wakisema:

"Amen!
Sifa na utukufu
na hekima na shukrani na heshima
na uweza na nguvu
viwe kwa Mungu wetu milele na
milele.
Amen!"

13 [i]Kisha mmoja wa wale wazee ishirini na
wanne akaniuliza, "Ni nani hawa waliovaa
mavazi meupe, nao wametoka wapi?"
14 [j]Nikamjibu, "Bwana, wewe wajua."
Naye akasema, "Hawa ni wale waliotoka
katika ile dhiki kuu, nao wamefua mavazi
yao katika damu ya Mwana-Kondoo na
kuyafanya meupe kabisa. 15 [k]Kwa hiyo,

"Wako mbele ya kiti cha enzi cha
Mungu
na kumtumikia usiku na mchana
katika hekalu lake;
naye aketiye katika kile kiti cha enzi
atatanda hema yake juu yao.
16 [l]Kamwe hawataona njaa
wala kiu tena.
Jua halitawapiga
wala joto lolote liunguzalo.
17 [m]Kwa maana Mwana-Kondoo
aliyeko katikati ya kile kiti cha
enzi
atakuwa Mchungaji wao;

[a]**7:1** Yer 49:36; Mt 24:31
[b]**7:2** Ufu 9:4; Mt 16:16
[c]**7:3** Ufu 6:6; Eze 9:4; Ufu 22:4
[d]**7:4** Ufu 9:16; 14:1-3
[e]**7:9** Ufu 5:9; 13:7; 7:15; Rum 11:25; Ufu 3:5; 6:11; 7:4
[f]**7:10** Za 3:8; Ufu 19:1
[g]**7:11** Ufu 4:4-10
[h]**7:12** Rum 11:36; Ufu 5:12-14
[i]**7:13** Ufu 3:4; 7:9
[j]**7:14** Ufu 22:14; Ebr 9:14; 1Yn 1:7
[k]**7:15** Ufu 22:3; 11:19; Isa 4:5-6
[l]**7:16** Isa 49:10
[m]**7:17** Za 23:1; Yn 10:11; Isa 51:11; Ufu 21:3

naye atawaongoza kwenda
kwenye chemchemi za maji yaliyo
hai.
Naye Mungu atafuta kila chozi
kutoka macho yao.”

*Lakiri Ya Saba Na Chetezo Cha Dhahabu*

8 [a]Mwana-Kondoo alipoivunja ile lakiri ya
saba, pakawa kimya mbinguni kwa muda
wa nusu saa.
2 [b]Nami nikawaona wale malaika saba
wanaosimama mbele za Mungu, nao
wakapewa tarumbeta saba.
3 [c]Malaika mwingine aliyekuwa na
chetezo cha dhahabu, akaja na kusimama
mbele ya madhabahu. Akapewa uvumba
mwingi ili autoe pamoja na maombi ya
watakatifu wote, juu ya yale madhabahu
ya dhahabu yaliyo mbele ya kile kiti cha
enzi. 4 [d]Ule moshi wa uvumba pamoja na
yale maombi ya watakatifu, vikapanda
juu mbele za Mungu, kutoka mkononi
mwa huyo malaika. 5 [e]Kisha yule malaika
akachukua kile chetezo, akakijaza moto
kutoka kwa yale madhabahu, akautupa juu
ya dunia. Pakatokea sauti za radi, ngurumo,
umeme wa radi na tetemeko la ardhi.

*Tarumbeta Ya Kwanza*

6 [f]Basi wale malaika saba waliokuwa na
zile tarumbeta saba wakajiandaa kuzipiga.
7 [g]Malaika wa kwanza akaipiga tarumbeta
yake, pakatokea mvua ya mawe na moto
uliochanganyika na damu, navyo vikatupwa
kwa nguvu juu ya nchi. Na theluthi ya dunia
ikateketea, theluthi ya miti ikateketea, na
nyasi yote mbichi ikateketea.

*Tarumbeta Ya Pili*

8 [h]Malaika wa pili akaipiga tarumbeta
yake na kitu kama mlima mkubwa
unaowaka moto kikatupwa baharini.
Theluthi ya bahari ikawa damu, 9 [i]theluthi
ya viumbe vyenye uhai viishivyo baharini
vikafa na theluthi ya meli zikaharibiwa.

*Tarumbeta Ya Tatu*

10 [j]Malaika wa tatu akaipiga tarumbeta
yake, na nyota kubwa iliyokuwa ikiwaka
kama taa ikaanguka toka angani, ikaangukia
theluthi ya mito na chemchemi za maji.
11 [k]Nyota hiyo inaitwa Uchungu. Theluthi
ya maji yakawa machungu na watu wengi
wakafa kutokana na maji hayo kwa maana
yalikuwa machungu.

*Tarumbeta Ya Nne*

12 [l]Kisha malaika wa nne akaipiga
tarumbeta yake, na theluthi ya jua, theluthi
ya mwezi na theluthi ya nyota zikapigwa.
Kwa hiyo theluthi moja ya mwanga ikawa
giza. Theluthi ya mchana ikawa haina
mwanga na pia theluthi ya usiku.
13 [m]Nilipokuwa tena nikitazama,
nikamsikia tai mmoja akipiga kelele kwa
sauti kuu wakati akiruka katikati ya mbingu,
akisema, “Ole! Ole! Ole wa watu waishio
duniani, kwa sababu ya tarumbeta ambazo
malaika hao wengine watatu wanakaribia
kuzipiga!”

*Tarumbeta Ya Tano*

9 [n]Malaika wa tano akaipiga tarumbeta
yake, nami nikaona nyota iliyokuwa
imeanguka toka angani hadi ardhini.
Nyota hiyo ilipewa ufunguo wa lile Shimo.[o]
2 [p]Alipolifungua hilo Shimo, moshi ukapanda
kutoka humo kama moshi wa tanuru kubwa
sana. Jua na anga vikatiwa giza na ule
moshi uliotoka katika hilo Shimo. 3 [q]Ndipo
katika ule moshi wakatoka nzige wakaenda
juu ya nchi, nao wakapewa nguvu kama

---

[a]**8:1** Ufu 6:1
[b]**8:2** Ufu 9:1, 13; 11:15; Mt 24:31; Ufu 8:6-13
[c]**8:3** Ufu 7:2; 5:8; Kut 30:1-6; Ebr 9:4
[d]**8:4** Za 141:2; Lk 1:10
[e]**8:5** Law 16:12-13; Ufu 4:5; 6:12
[f]**8:6** Ufu 8:2
[g]**8:7** Eze 38:22; Ufu 9:15-18; 12:4; 9:4
[h]**8:8** Yer 51:25; 16:3
[i]**8:9** Ufu 8:7; 16:3
[j]**8:10** Isa 14:12; Ufu 9:1; 14:7; 16:4
[k]**8:11** Yer 9:15; 23:15
[l]**8:12** Kut 10:21-23; Ufu 6:12-13
[m]**8:13** Ufu 14:6; 19:17; 11:14; 12:12
[n]**9:1** Ufu 8:10; Lk 8:31
[o]1 Yaani Abyss kwa Kiyunani; maana yake ni Kuzimu, yaani makao ya pepo wachafu.
[p]**9:2** Mwa 19:28; Kut 19:18; Yoe 2:2-10
[q]**9:3** Kut 10:12-15

zile za nge wa duniani. 4 [a]Wakaambiwa wasidhuru nyasi ya nchi, wala mmea wala mti wowote, bali wawadhuru tu wale watu ambao hawana muhuri wa Mungu kwenye vipaji vya nyuso zao. 5 [b]Wakaruhusiwa kuwatesa kwa muda wa miezi mitano, lakini wasiwaue. Uchungu wa kuuma kwao ulikuwa kama ule wa mtu aumwapo na nge. 6 [c]Katika siku hizo watu watatafuta kifo lakini hawatakiona, watatamani kufa, lakini kifo kitawakimbia.

7 [d]Wale nzige walikuwa na umbo kama la farasi waliotayarishwa kwa ajili ya vita. Kwenye vichwa vyao kulikuwa na kitu kama taji za dhahabu na nyuso zao zilikuwa kama za binadamu. 8 [e]Walikuwa na nywele kama za wanawake, na meno yao yalikuwa kama ya simba. 9 [f]Walikuwa na dirii kama za chuma, na sauti za mabawa yao zilikuwa kama ngurumo za farasi wengi na magari mengi yakikimbilia vitani. 10 [g]Walikuwa na mikia yenye miiba ya kuumia kama nge. Nguvu yao ya kutesa watu kwa huo muda wa miezi mitano ilikuwa katika hiyo mikia yao. 11 [h]Walikuwa na mfalme wao, ambaye ni malaika wa lile Shimo, ambaye jina lake kwa Kiebrania ni Abadoni, na kwa Kiyunani ni Apolioni.[i]

12 [j]Ole ya kwanza imepita, bado nyingine mbili zinakuja.

*Tarumbeta Ya Sita*

13 [k]Malaika wa sita akaipiga tarumbeta yake, nami nikasikia sauti ikitoka katika zile pembe za madhabahu ya dhahabu iliyoko mbele za Mungu. 14 [l]Ile sauti ikamwambia yule malaika wa sita mwenye tarumbeta, "Wafungulie wale malaika wanne waliofungwa kwenye ule mto mkubwa Frati." 15 [m]Basi wale malaika wanne, waliokuwa wamewekwa tayari kwa ajili ya saa hiyo, na siku hiyo, na mwezi huo, na mwaka huo ili wawaue theluthi ya wanadamu wakafunguliwa. 16 [n]Idadi ya majeshi wapanda farasi ilikuwa 200,000,000. Nilisikia idadi yao.

17 [o]Hivi ndivyo nilivyowaona hao farasi na wapanda farasi katika maono yangu: Wapanda farasi walivaa dirii vifuani zenye rangi nyekundu sana kama ya moto na yakuti samawi na kiberiti. Vichwa vya hao farasi vilikuwa kama vichwa vya simba, na moto, moshi na kiberiti vilitoka vinywani mwao. 18 [p]Theluthi ya wanadamu wakauawa kwa mapigo hayo matatu, yaani, huo moto, moshi na kiberiti, vilivyotoka kwenye vinywa vya hao farasi. 19 [q]Nguvu za hao farasi zilikuwa katika vinywa vyao na kwenye mikia yao, kwa sababu mikia yao ilikuwa kama nyoka, yenye vichwa ambayo waliitumia kudhuru.

20 [r]Wanadamu waliosalia, ambao hawakuuawa katika mapigo hayo, bado walikataa kutubia kazi za mikono yao na hawakuacha kuabudu mashetani na sanamu za dhahabu, za fedha, za shaba, za mawe na za miti, ambazo haziwezi kuona, kusikia wala kutembea. 21 [s]Wala hawakutubu na kuacha matendo yao ya uuaji, uchawi, uasherati wala wizi wao.

*Malaika Mwenye Kitabu Kidogo*

10 [t]Kisha nikamwona malaika mwingine mwenye nguvu akishuka kutoka mbinguni. Alikuwa amevikwa wingu na upinde wa mvua juu ya kichwa chake. Uso wake uling'aa kama jua na miguu yake

[a]**9:4** Ufu 7:2-3; 6:6; 8:7; Eze 9:4; Ufu 7:3
[b]**9:5** Ufu 9:3, 10
[c]**9:6** Ay 7:15; Ufu 6:16
[d]**9:7** Yoe 2:4; Dan 7:8
[e]**9:8** Yoe 1:6
[f]**9:9** Yoe 2:5
[g]**9:10** Ufu 9:3, 5, 19
[h]**9:11** Ufu 9:1, 2; Lk 8:31; 16:16; Ay 26:6; 28:22
[i]11 Abadoni au Apolioni maana yake ni Mharabu, yaani Yule aharibuye.
[j]**9:12** Ufu 8:13
[k]**9:13** Kut 30:1-3; Ufu 8:3
[l]**9:14** Ufu 16:12
[m]**9:15** Ufu 20:7; 8:7; 9:12
[n]**9:16** Ufu 5:11; 7:4
[o]**9:17** Ufu 11:5
[p]**9:18** Ufu 8:7; 9:15, 17
[q]**9:19** Isa 9:15
[r]**9:20** Mik 5:13; Mdo 7:41; 1Kor 10:20; Dan 5:23
[s]**9:21** Ufu 2:21; 18:23; 17:2-5
[t]**10:1** Ufu 5:2; Mt 17:2; Ufu 1:16; 1:15

ilikuwa kama nguzo za moto. 2 [a]Mkononi
mwake alikuwa ameshika kijitabu
kilichokuwa kimefunguliwa. Akauweka
mguu wake wa kuume juu ya bahari na
mguu wake wa kushoto akauweka juu ya
nchi kavu. 3 [b]Naye akapiga kelele kwa sauti
kuu kama simba anayenguruma. Alipopiga
kelele, zile radi saba zikatoa ngurumo zake.
4 [c]Nazo zile radi saba zilipotoa ngurumo,
nilitaka kuanza kuandika, lakini nikasikia
sauti kutoka mbinguni ikisema, "Yatie
muhuri hayo yaliyosemwa na hizo radi
saba na usiyaandike."

5 [d]Kisha yule malaika niliyekuwa
nimemwona akiwa amesimama juu ya
bahari na juu ya nchi akainua mkono wake
wa kuume kuelekea mbinguni. 6 [e]Naye
akaapa kwa Yule aishiye milele na milele,
aliyeumba mbingu na vyote vilivyomo,
dunia na vyote viijazavyo, pamoja na
bahari na vyote vilivyomo ndani yake,
akasema, "Hakuna kungoja tena! 7 [f]Lakini
katika siku zile ambazo huyo malaika wa
saba atakapokaribia kuipiga hiyo tarumbeta
yake, siri ya Mungu itatimizwa, kama
vile alivyowatangazia watumishi wake
manabii."

8 Ndipo ile sauti niliyokuwa nimeisikia
kutoka mbinguni ikasema nami tena
ikaniambia, "Nenda, chukua kile kitabu
kilichofunguliwa kilichoko mkononi mwa
yule malaika aliyesimama juu ya bahari na
juu ya nchi kavu."

9 [g]Basi nikamwendea nikamwomba
yule malaika anipe kile kitabu kidogo.
Akaniambia, "Chukua na ukile. Kitakuwa
kichungu tumboni mwako, lakini kinywani
mwako kitakuwa kitamu kama asali."
10 [h]Hivyo nikakichukua kile kitabu kidogo
kutoka mkononi mwa yule malaika
nikakila. Kilikuwa kitamu kama asali
kinywani mwangu, lakini baada ya kukila,
tumbo langu likatiwa uchungu. 11 [i]Kisha
nikaambiwa, "Imekupasa kutoa unabii tena
kuhusu makabila mengi, mataifa, lugha na
wafalme."

*Mashahidi Wawili*

11 [j]Ndipo nikapewa mwanzi uliokuwa
kama ufito wa kupimia, nikaambiwa,
"Nenda ukapime hekalu la Mungu pamoja
na madhabahu, nawe uwahesabu wale
waabuduo humo. 2 [k]Lakini usiupime ua
wa nje wa Hekalu, uache, kwa sababu ua
huo wamepewa watu wa Mataifa. Hao
wataukanyagakanyaga mji mtakatifu
kwa muda wa miezi arobaini na miwili.
3 [l]Nami nitawapa mashahidi wangu wawili
uwezo, nao watoe unabii kwa muda wa siku
1,260, wakiwa wamevaa nguo za gunia."
4 [m]Hawa ndio ile mizeituni miwili na vile
vinara viwili vya taa visimamavyo mbele
za Bwana Mungu wa dunia yote. 5 [n]Kama
mtu yeyote akitaka kuwadhuru, moto
hutoka vinywani mwao na kuwateketeza
adui zao. Hivi ndivyo impasavyo kufa mtu
yeyote atakayetaka kuwadhuru. 6 [o]Watu
hawa wanao uwezo wa kufunga anga ili
mvua isinyeshe wakati wote watakapokuwa
wanatoa unabii wao. Nao watakuwa na
uwezo wa kuyabadili maji kuwa damu na
kuipiga dunia kwa kila aina ya mapigo
mara kwa mara kama watakavyo.

7 [p]Basi watakapokuwa wamemaliza
ushuhuda wao, yule mnyama atokaye katika
lile Shimo atapigana nao vita, atawashinda
na kuwaua. 8 [q]Maiti zao zitabaki katika
barabara ya mji mkubwa,[r] ambao kwa

---

[a]**10:2** Ufu 10:8-10; 5:1; 10:5, 8
[b]**10:3** Ufu 4:5; Hos 11:10; Yer 25:30; Amo 1:2
[c]**10:4** Dan 8:26; Ufu 22:10
[d]**10:5** Dan 12:7
[e]**10:6** Ufu 4:11; 16:17
[f]**10:7** Rum 16:25
[g]**10:9** Yer 15:16; Eze 2:8; 3:3
[h]**10:10** Ufu 10:9; Eze 3:3; 2:10
[i]**10:11** Eze 40:3; Ufu 21:15; 12:3; 11:19; Mwa 37:9
[j]**11:1** Eze 40:3; Ufu 21:15; 12:3; 11:19; Mwa 37:9
[k]**11:2** Eze 40:17, 20; Lk 21:24; Ufu 21:2; Dan 12:7; Ufu 13:5
[l]**11:3** Ufu 1:5; 2:13; Neh 9:1; Yon 3:5
[m]**11:4** Za 52:8; Yer 11:16; Zek 4:14
[n]**11:5** 2Sam 22:9; Ufu 9:17, 18; Hes 16:29, 35
[o]**11:6** Kut 7:17, 19; Ufu 8:8; Mt 2:13; Ufu 12:5
[p]**11:7** Ufu 13:1-4; 13:7; Dan 7:21; 10:13, 21; 12:1; Yud 9; Mt 25:41
[q]**11:8** Yer 23:14; Eze 16:46; Hes 13:12
[r]8 Mji mkubwa hapa inamaanisha Yerusalemu ambako Bwana wao alisulubiwa.

fumbo unaitwa Sodoma na Misri,[a] ambapo
pia Bwana wao alisulubiwa. 9 [b]Kwa muda
wa siku tatu na nusu, watu wa kila kabila,
jamaa, lugha na taifa wataziangalia hizo
maiti zao na hawataruhusu wazikwe.
10 [c]Watu waishio duniani watazitazama
kwa furaha maiti za hao manabii wawili
na kushangilia kwa kupeana zawadi kwa
sababu hao manabii waliwatesa watu
waishio duniani.
11 [d]Lakini baada ya zile siku tatu na
nusu, pumzi ya uhai kutoka kwa Mungu
ikawaingia, nao wakasimama kwa miguu
yao na wote waliowaona wakaingiwa na
hofu kuu. 12 [e]Kisha wale manabii wawili
wakasikia sauti kuu kutoka mbinguni
ikiwaambia, "Njooni huku juu!" Nao
wakapaa mbinguni katika wingu, wakati
adui zao wakiwa wanawatazama.
13 [f]Saa iyo hiyo, kukatokea tetemeko
kubwa la nchi na sehemu ya kumi ya mji
ikaanguka. Watu elfu saba wakauawa
katika tetemeko hilo, nao walionusurika
wakaogopa sana, wakamtukuza Mungu wa
mbinguni.
14 [g]Ole ya pili imekwisha kupita, tazama
ole ya tatu inakuja upesi.

### *Tarumbeta Ya Saba*

15 [h]Yule malaika wa saba akaipiga
tarumbeta yake, pakawa na sauti kubwa
mbinguni iliyosema:

"Ufalme wa ulimwengu umekuwa
ufalme wa Bwana wetu na wa
Kristo wake,
naye atatawala milele na milele."

16 [i]Nao wale wazee ishirini na wanne,
waliokuwa wameketi mbele za Mungu,
kwenye viti vyao vya enzi, wakaanguka
kifudifudi, wakamwabudu Mungu,
17 [j]wakisema:

"Tunakushukuru, BWANA Mungu
Mwenyezi,
uliyeko na uliyekuwako,
kwa kuwa umetwaa uweza wako
mkuu
na ukaanza kutawala.
18 [k]Mataifa walikasirika nao
wakati wa ghadhabu yako
umewadia.
Wakati umewadia wa kuwahukumu
waliokufa
na kuwapa thawabu watumishi
wako manabii
na watakatifu wako pamoja na wale
wote
wanaoliheshimu Jina lako,
wakubwa kwa wadogo:
na kuwaangamiza wale
wanaoiangamiza dunia."

19 [l]Ndipo hekalu la Mungu lililoko
mbinguni likafunguliwa, na sanduku la
agano lake likaonekana humo ndani.
Kukatokea mianga ya umeme wa radi,
ngurumo, sauti za radi, tetemeko la nchi
na mvua kubwa ya mawe.

### *Mwanamke Na Joka*

12 Kukaonekana ishara kuu mbinguni:
Palikuwa na mwanamke aliyevikwa
jua, na mwezi ukiwa chini ya miguu yake,
na taji ya nyota kumi na mbili ilikuwa
kichwani mwake. 2 [m]Alikuwa na mimba
naye akilia kwa uchungu kwa kuwa alikuwa
anakaribia kuzaa. 3 [n]Kisha ishara nyingine
ikaonekana mbinguni: Likaonekana joka
kubwa jekundu lenye vichwa saba na
pembe kumi na taji saba katika vichwa
vyake. 4 [o]Mkia wake ukakokota theluthi
ya nyota zote angani na kuziangusha

[a]8 Sodoma na Misri hapa inamaanisha Yerusalemu, kwa sababu mataifa watafanya uovu mwingi wa kila aina katika kipindi hicho cha miaka mitatu na nusu.
[b]**11:9** Za 79:2, 3
[c]**11:10** Ufu 3:10; Neh 8:10, 12; Es 9:19, 22
[d]**11:11** Ufu 3:10; Neh 8:10, 12, 14
[e]**11:12** Ufu 4:1; 2Fal 2:11; Mdo 1:9
[f]**11:13** Ufu 6:12; 16:9; 19:7; 16:11; 12:3
[g]**11:14** Ufu 8:13
[h]**11:15** Mt 24:31; Ufu 10:7; 6:10; 16:17; 19:1; 12:10; Za 145:13; Lk 1:33; Ufu 12:9
[i]**11:16** Ufu 4:4
[j]**11:17** Ufu 1:8; 19:6
[k]**11:18** Za 2:1; Ufu 10:7; 19:5
[l]**11:19** Ufu 15:5, 8; 16:21
[m]**12:2** Gal 4:19
[n]**12:3** Dan 7:7, 20; Ufu 13:1; 19:21
[o]**12:4** Ufu 8:7; Dan 8:10; Mt 22:16

katika nchi. Ndipo lile joka likasimama mbele ya yule mwanamke aliyekuwa karibu kuzaa ili lipate kumla huyo mtoto mara tu atakapozaliwa.
5 [a]Yule mwanamke akazaa mtoto mwanaume, atakayeyatawala mataifa yote kwa fimbo yake ya utawala ya chuma. Lakini huyo mtoto akanyakuliwa na kupelekwa kwa Mungu kwenye kiti chake cha enzi.
6 [b]Yule mwanamke akakimbilia jangwani, ambako Mungu alikuwa amemtayarishia mahali ili apate kutunzwa huko kwa muda wa siku 1,260.

*Malaika Mikaeli Amshinda Yule Joka*

7 Basi palikuwa na vita mbinguni: Mikaeli na malaika zake wakapigana na hilo joka, nalo joka pamoja na malaika zake likapigana nao.
8 Lakini joka na malaika zake wakashindwa, na hapakuwa tena na nafasi yao huko mbinguni.
9 [c]Lile joka kuu likatupwa chini, yule nyoka wa zamani aitwaye ibilisi au Shetani, aupotoshaye ulimwengu wote. Akatupwa chini duniani, yeye pamoja na malaika zake.

*Ushindi Mbinguni Watangazwa*

10 [d]Kisha nikasikia sauti kuu mbinguni, ikisema:

"Sasa wokovu na uweza na Ufalme
wa Mungu wetu umekuja
na mamlaka ya Kristo wake.
Kwa kuwa ametupwa chini
mshtaki wa ndugu zetu,
anayewashtaki mbele za Mungu
usiku na mchana.
11 [e]Nao wakamshinda
kwa damu ya Mwana-Kondoo
na kwa neno la ushuhuda wao.
Wala wao hawakuyapenda maisha
yao
hata kufa.
12 [f]Kwa hiyo, furahini ninyi mbingu
na wote wakaao humo!
Lakini ole wenu nchi na bahari,
kwa maana huyo ibilisi ameshuka
kwenu,
akiwa amejaa ghadhabu,
kwa sababu anajua ya kuwa
muda wake ni mfupi!"

13 Lile joka lilipoona kuwa limetupwa chini duniani, lilimfuatilia yule mwanamke aliyekuwa amezaa mtoto mwanaume.
14 [g]Lakini huyo mwanamke akapewa mabawa mawili ya tai mkubwa, kusudi aweze kuruka mpaka mahali palipotayarishwa kwa ajili yake huko jangwani, ambako atatunzwa kwa wakati na nyakati na nusu,[h] ya wakati ambako yule joka hawezi kufika.
15 Ndipo lile joka likamwaga maji kama mto kutoka kinywani mwake, ili kumfikia huyo mwanamke na kumkumba kama mafuriko.
16 Lakini nchi ikamsaidia huyo mwanamke kwa kufungua kinywa na kuumeza huo mto ambao huyo joka alikuwa ameutoa kinywani mwake.
17 [i]Kisha lile joka likapatwa na hasira kali kwa ajili ya huyo mwanamke na likaondoka ili kupigana vita na watoto waliosalia wa huyo mwanamke, yaani, wale wanaozitii amri za Mungu na kuushika ushuhuda wa Yesu Kristo.
13 [j]Yule joka akajikita katika mchanga ulioko ufuoni mwa bahari.

*Mnyama Kutoka Baharini*

Nami nikamwona mnyama akitoka ndani ya bahari. Mnyama huyo alikuwa na pembe kumi na vichwa saba, akiwa na taji kumi kwenye hizo pembe zake, na juu ya kila kichwa kulikuwa na jina la kukufuru.
2 [k]Mnyama yule niliyemwona alifanana na chui, lakini miguu yake ilikuwa kama ya dubu na kichwa chake kama cha simba. Lile joka likampa huyo mnyama nguvu zake, kiti chake cha enzi na mamlaka makubwa.
3 [l]Kimojawapo ya

[a] **12:5** Za 2:9; Ufu 19:15
[b] **12:6** Ufu 11:2
[c] **12:9** Mwa 3:1-7; Mt 25:41; Ufu 20:3, 8, 10; Lk 10:18; Yn 12:31
[d] **12:10** Ufu 11:15; Zek 3:1
[e] **12:11** Ufu 7:14; 6:9; Lk 14:26
[f] **12:12** Isa 44:23; Ufu 18:20; 8:13; 10:6
[g] **12:14** Kut 19:4; Dan 7:25
[h] 14 Maana yake ni miaka mitatu na nusu.
[i] **12:17** Ufu 11:7; Mwa 3:15; Ufu 14:12; 1:2
[j] **13:1** Dan 7:1-6; Ufu 16:13; 12:3; Dan 11:36; Ufu 17:3
[k] **13:2** Dan 7:6; 7:5; 7:4; Ufu 16:10
[l] **13:3** Ufu 17:8

vichwa vya huyo mnyama kilikuwa kama
kilichokwisha kupata jeraha la mauti, lakini
jeraha hilo la mauti likapona. Ulimwengu
wote ukashangaa ukamfuata huyo mnyama.
4 [a]Watu wakaliabudu lile joka kwa sababu
lilikuwa limempa huyo mnyama mamlaka
yake, pia wakamwabudu huyo mnyama na
kuuliza, "Ni nani aliye kama huyu mnyama?
Ni nani awezaye kupigana vita naye?"
5 [b]Huyo mnyama akapewa kusema
maneno ya kiburi na kukufuru na kutumia
mamlaka yake kwa muda wa miezi arobaini
na miwili. 6 [c]Akafungua kinywa chake ili
kumkufuru Mungu, akilitukana Jina lake na
mahali aishipo na wale wakaao mbinguni.
7 [d]Pia akaruhusiwa kufanya vita na
watakatifu na kuwashinda. Akapewa uwezo
juu ya watu wa kila kabila, jamaa, lugha
na taifa. 8 [e]Nao watu wote waishio duniani
watamwabudu huyo mnyama, yaani, wale
wote ambao majina yao hayakuandikwa
kwenye kitabu cha uzima cha Mwana-
Kondoo aliyechinjwa tangu kuumbwa kwa
ulimwengu.
9 [f]Yeye aliye na sikio na asikie.

10 [g]Ikiwa mtu ni wa kuchukuliwa
mateka,
atachukuliwa mateka.
Ikiwa mtu ni wa kuuawa kwa
upanga,
atauawa kwa upanga.

Hapa ndipo penye wito wa subira na imani
ya watakatifu.

*Mnyama Kutoka Dunia*

11 [h]Kisha nikamwona mnyama mwingine,
akipanda juu kutoka dunia. Alikuwa
na pembe mbili kama mwana-kondoo,
lakini akanena kama joka. 12 [i]Akatumia
mamlaka yote ya yule mnyama wa
kwanza kwa niaba yake, naye akawafanya
wote wakaao duniani kumwabudu yule
mnyama wa kwanza, ambaye jeraha lake
la mauti lilipona. 13 [j]Naye akafanya ishara
kuu na za ajabu, hata kusababisha moto
kushuka toka mbinguni kuja duniani watu
wakiona waziwazi. 14 [k]Kwa sababu ya zile
ishara alizokuwa amepewa uwezo wa
kuzifanya kwa niaba ya yule mnyama wa
kwanza, akawadanganya wakaao duniani.
Akawaamuru wasimamishe sanamu kwa
heshima ya yule mnyama aliyekuwa
amejeruhiwa kwa upanga lakini akaishi.
15 [l]Akapewa uwezo wa kuipa pumzi ile
sanamu ya yule mnyama wa kwanza, ili
iweze kusema na kuwasababisha wale wote
waliokataa kuiabudu hiyo sanamu kuuawa.
16 [m]Pia alimlazimisha kila mmoja, mdogo
na mkubwa, tajiri na maskini, mtu huru na
mtumwa, atiwe chapa kwenye mkono wake
wa kuume au kwenye kipaji chake cha uso,
17 [n]ili kwamba mtu yeyote asiweze kununua
wala kuuza isipokuwa amekuwa na hiyo
chapa, ambayo ni jina la huyo mnyama au
tarakimu za jina lake.
18 [o]Hapa ndipo penye hekima. Yeye
aliye na ufahamu na ahesabu tarakimu za
huyo mnyama, kwa maana ni tarakimu za
kibinadamu. Tarakimu zake ni 666.

*Mwana-Kondoo Na Wale 144,000*

14 [p]Kisha nikatazama na hapo mbele
yangu alikuwepo Mwana-Kondoo,
akiwa amesimama juu ya Mlima Sayuni.
Pamoja naye walikuwa wale 144,000
wenye Jina la Mwana-Kondoo na Jina la
Baba yake likiwa limeandikwa kwenye
vipaji vya nyuso zao. 2 [q]Nami nikasikia
sauti kutoka mbinguni kama sauti ya maji
mengi yaendayo kwa kasi na sauti kama
ngurumo ya radi. Sauti hiyo niliyoisikia
ilikuwa kama sauti ya wapiga vinubi

[a]**13:4** Kut 15:11
[b]**13:5** Dan 11:36; 2The 2:4; Ufu 11:2
[c]**13:6** Ufu 12:12
[d]**13:7** Dan 7:21; Ufu 11:7; 5:9
[e]**13:8** Ufu 3:10; 3:5; 20:12; Mt 25:34
[f]**13:9** Ufu 2:7
[g]**13:10** Yer 15:2; 43:11; Hes 6:12; Ufu 14:12
[h]**13:11** Ufu 13:1, 2
[i]**13:12** Ufu 19:20; 20:4
[j]**13:13** Mt 24:24; 2Fal 1:10; Lk 9:54
[k]**13:14** 2The 2:9, 10; Ufu 12:9
[l]**13:15** Dan 3:3-6
[m]**13:16** Ufu 19:5; 14:9
[n]**13:17** Ufu 14:9; 14:11; 15:2
[o]**13:18** Ufu 17:9; 15:2; 21:17
[p]**14:1** Ufu 5:6; Za 2:6; Ufu 7:4; 3:12
[q]**14:2** Ufu 1:15; 5:8-9; Eze 1:24; 43:2

wakipiga vinubi vyao. [3] [a]Nao wakaimba
wimbo mpya mbele ya hicho kiti cha enzi
na mbele ya wale viumbe wanne wenye
uhai na wale wazee. Hakuna mtu yeyote
aliyeweza kujifunza wimbo huo isipokuwa
hao 144,000 waliokuwa wamekombolewa
kutoka duniani. [4] [b]Hawa ndio wale ambao
hawakujitia unajisi kwa wanawake,
kwa kuwa wao ni bikira. Wao humfuata
Mwana-Kondoo kila aendako. Hawa
wamekombolewa kutoka miongoni mwa
wanadamu wakawa malimbuko kwa Mungu
na kwa Mwana-Kondoo. [5] [c]Vinywani mwao
hapakuonekana uongo, wala hawakuwa na
hatia yoyote.

*Malaika Watatu*

[6] [d]Kisha nikamwona malaika mwingine
akiruka juu angani, naye alikuwa na Injili
ya milele ya kuwatangazia wale waishio
duniani, yaani, kwa kila taifa, kabila, lugha
na jamaa. [7] [e]Akasema kwa sauti kubwa,
“Mcheni Mungu na kumpa utukufu, kwa
maana saa ya hukumu yake imewadia.
Mwabuduni yeye aliyeziumba mbingu,
dunia, bahari na chemchemi za maji.”

[8] [f]Malaika wa pili akafuata akisema,
“Umeanguka! Umeanguka Babeli Mkuu,
ule uliyafanya mataifa yote kulewa kwa
mvinyo wa ghadhabu ya uasherati wake.”

[9] [g]Malaika wa tatu akawafuata hao
wawili akisema kwa sauti kubwa, “Kama
mtu yeyote anamwabudu huyo mnyama
na sanamu yake na kutiwa chapa yake
kwenye kipaji chake cha uso au kwenye
mkono wake, [10] [h]yeye pia atakunywa
mvinyo wa hasira kali ya Mungu ambayo
imemiminwa katika kikombe cha ghadhabu
yake pasipo kuchanganywa na maji. Naye
atateswa kwa moto uwakao na kiberiti
mbele ya malaika watakatifu na mbele za
Mwana-Kondoo. [11] [i]Nao moshi wa mateso
yao hupanda juu milele na milele. Hakuna
mapumziko, mchana wala usiku, kwa wale
wamwabuduo huyo mnyama na sanamu
yake, au kwa yeyote anayepokea chapa ya
jina lake.” [12] [j]Hapa ndipo penye wito wa
subira na uvumilivu wa watakatifu; wale
wanaozishika amri za Mungu na kudumu
katika uaminifu kwa Yesu.

[13] [k]Kisha nikasikia sauti kutoka mbinguni
ikisema, “Andika: Wamebarikiwa wafu
wafao katika Bwana tangu sasa.”

“Naam,” asema Roho, “watapumzika
kutoka taabu zao, kwa kuwa matendo yao
yatawafuata.”

*Kuvuna Mavuno Ya Dunia*

[14] [l]Nikatazama, hapo mbele yangu
palikuwa na wingu jeupe, na aliyekuwa
ameketi juu ya hilo wingu alikuwa “kama
Mwana wa Adamu” mwenye taji ya dhahabu
kichwani mwake na mundu mkali mkononi
mwake. [15] [m]Kisha malaika mwingine akaja
kutoka hekaluni naye akamwita kwa sauti
kubwa yule aliyekuwa ameketi juu ya lile
wingu akasema, “Chukua mundu wako
ukavune kwa kuwa wakati wa mavuno
umewadia, kwa maana mavuno ya dunia
yamekomaa.” [16] Hivyo yule aliyekuwa
ameketi juu ya lile wingu akauzungusha
mundu wake duniani, nayo dunia ikavunwa.

[17] [n]Malaika mwingine akatoka katika
hekalu lililoko mbinguni, naye pia
alikuwa na mundu mkali. [18] [o]Kisha malaika
mwingine, aliyekuwa na mamlaka juu ya
moto, akatoka kwenye madhabahu, naye
akamwita yule malaika mwenye mundu
mkali kwa sauti kubwa, akisema, “Chukua
mundu wako mkali ukakusanye vichala
vya mizabibu ya dunia, maana zabibu
zake zimeiva.” [19] [p]Hivyo yule malaika

---

[a]**14:3** Ufu 5:9; 4:6; 4:4; 14:1
[b]**14:4** 2Kor 11:2; Ufu 3:4; Yak 1:18
[c]**14:5** Yn 1:47; Efe 5:27
[d]**14:6** Ufu 8:13; 19:17; 3:10; 13:7
[e]**14:7** Za 34:9; Ufu 15:4; 11:13; 8:10
[f]**14:8** Isa 21:9; Ufu 17:2-4; 18:3
[g]**14:9** Ufu 13:14
[h]**14:10** Isa 51:17; Yer 25:15; 51:7
[i]**14:11** Isa 34:10; Ufu 19:3
[j]**14:12** Ufu 13:10; 1Kor 15:18; 1The 4:16; 1Kor 15:18; 1The 4:16
[k]**14:13** 1Kor 15:18; 1The 4:16; Ufu 2:7; 22:17
[l]**14:14** Dan 7:13; Ufu 1:13; 6:2
[m]**14:15** Yoe 3:13; Mk 4:29; Yer 51:33
[n]**14:17** Ufu 14:15
[o]**14:18** Ufu 6:9; 8:5; 16:7; 14:15
[p]**14:19** Ufu 19:15

akauzungusha mundu wake duniani na
kukusanya zabibu za dunia na kuzitupa
kwenye shinikizo kubwa la ghadhabu ya
Mungu. 20 [a]Lile shinikizo likakanyagwa
nje ya mji, nayo damu ikatiririka kama
mafuriko kutoka hilo shinikizo kufikia
kimo cha hatamu za farasi,[b] kwa umbali
wa maili 200.[c]

*Malaika Saba Na Mapigo Saba*

15 [d]Ndipo nikaona ishara nyingine kubwa
ya ajabu mbinguni: malaika saba
wenye yale mapigo saba ya mwisho, kwa
sababu kwa mapigo hayo ghadhabu ya
Mungu ilikuwa imekamilika. 2 [e]Nikaona
kile kilichoonekana kama bahari ya kioo
iliyochanganyikana na moto. Kando ya
hiyo bahari, walikuwa wamesimama wale
watu waliomshinda yule mnyama na
sanamu yake pamoja na tarakimu ya jina
lake. Mikononi mwao walikuwa wameshika
vinubi walivyopewa na Mungu. 3 [f]Nao
wakaimba wimbo wa Mose, mtumishi wa
Mungu, na wimbo wa Mwana-Kondoo,
wakisema:

“BWANA Mungu Mwenyezi,
matendo yako ni makuu na ya
ajabu.
Njia zako wewe ni za haki na za
kweli,
Mfalme wa nyakati zote!
4 [g]Ni nani ambaye hatakuogopa wewe
Bwana
na kulitukuza jina lako?
Kwa kuwa wewe peke yako ndiwe
mtakatifu.
Mataifa yote yatakuja
na kuabudu mbele zako,
kwa kuwa matendo yako ya haki
yamedhihirishwa.”

5 [h]Baada ya haya nikatazama, nalo
hekalu, la hema la Ushuhuda, lilikuwa
limefunguliwa mbinguni. 6 [i]Ndani ya lile
hekalu wakatoka malaika saba wakiwa na
mapigo saba. Walikuwa wamevaa nguo safi
za kitani ing’aayo na kufungwa mikanda ya
dhahabu vifuani mwao. 7 [j]Ndipo mmoja wa
wale viumbe wanne wenye uhai akawapa
wale malaika saba mabakuli saba ya
dhahabu yaliyojaa ghadhabu ya Mungu,
yeye aishiye milele na milele. 8 [k]Nalo lile
hekalu lilijawa na moshi uliotokana na
utukufu wa Mungu na uweza wake, wala
hakuna yeyote aliyeweza kuingia mle
hekaluni mpaka yale mapigo saba ya wale
malaika saba yalipomalizika.

*Mabakuli Saba Ya Ghadhabu Ya Mungu*

16 [m]Kisha nikasikia sauti kubwa kutoka
mle Hekaluni ikiwaambia wale malaika
saba, “Nendeni, mkayamwage duniani hayo
mabakuli saba ya ghadhabu ya Mungu.”
2 [n]Malaika wa kwanza akaenda
akalimwaga hilo bakuli lake juu ya nchi.
Majipu mabaya yenye maumivu makali
yakawapata wale watu wote waliokuwa
na chapa ya yule mnyama na walioabudu
sanamu yake.
3 [o]Malaika wa pili akalimwaga bakuli
lake baharini, nayo ikabadilika kuwa damu
kama ya mtu aliyekufa na kila kiumbe hai
kilichokuwa ndani ya bahari kikafa.
4 [p]Malaika wa tatu akalimwaga bakuli
lake katika mito na chemchemi za maji,
nazo zikawa damu. 5 [q]Ndipo nikamsikia
malaika msimamizi wa maji akisema:

[a]**14:20** Yoe 3:13; Ebr 13:12; Ufu 11:8
[b]20 Kimo cha hatamu za farasi ni kama mita moja na nusu.
[c]20 Maili 200 ni sawa na kilomita 320.
[d]**15:1** Ufu 12:1-3; 17:1; 21:9; Law 26:21
[e]**15:2** Ufu 4:6; 13:14
[f]**15:3** Kut 15:1; Kum 32:4; Za 111:2; 145:17
[g]**15:4** Yer 10:7; Isa 66:23
[h]**15:5** Ufu 11:19; Hes 1:50
[i]**15:6** Ufu 14:15; 1:13
[j]**15:7** Ufu 4:6
[k]**15:8** Isa 6:4; 1Fal 8:10-11; 2Nya 5:13-14
[m]**16:1** Ufu 15:1; 11:19; 15:1; 16:2-21; Za 79:6; Sef 3:8
[n]**16:2** Ufu 8:7; 13:15; 17; Kut 9:9-11
[o]**16:3** Kut 7:17-21; Ufu 6:11
[p]**16:4** Ufu 8:10
[q]**16:5** Ufu 15:3-4; 15:3; 1:4; 15:4; 6:10

"Wewe una haki katika hukumu hizi
ulizotoa,
wewe uliyeko, uliyekuwako, Uliye
Mtakatifu,
kwa sababu umehukumu hivyo;
6 [a]kwa kuwa walimwaga damu ya
watakatifu wako
na manabii wako,
nawe umewapa damu wanywe
kama walivyostahili."

7 [b]Nikasikia madhabahu ikiitikia,

"Naam, BWANA Mungu Mwenyezi,
hukumu zako ni kweli na haki."

8 [c]Malaika wa nne akamimina bakuli
lake kwenye jua, nalo likapewa nguvu
za kuwaunguza watu kwa moto. 9 [d]Watu
wakaunguzwa na hilo joto kali, wakalaani
Jina la Mungu, aliyekuwa na uwezo juu ya
mapigo haya, tena wakakataa kutubu na
kumtukuza Mungu.
10 [e]Malaika wa tano akamimina bakuli
lake kwenye kiti cha enzi cha yule mnyama,
nao ufalme wake ukagubikwa na giza.
Watu wakatafuna ndimi zao kwa ajili
ya maumivu, 11 [f]wakamlaani Mungu wa
mbinguni kwa sababu ya maumivu na
majeraha yao, wala hawakutubu kwa ajili
ya matendo yao maovu.
12 [g]Malaika wa sita akamimina bakuli
lake kwenye mto mkubwa Frati, maji
yake yakakauka ili kutayarisha njia kwa
ajili ya wafalme watokao Mashariki.
13 [h]Kisha nikaona roho wachafu watatu
waliofanana na vyura wakitoka katika
kinywa cha lile joka na katika kinywa
cha yule mnyama na katika kinywa cha
yule nabii wa uongo. 14 [i]Hizo ndizo roho
za pepo wachafu zitendazo miujiza. Nazo
huwaendea wafalme wa ulimwengu wote
na kuwakusanya tayari kwa ajili ya vita
katika siku ile kuu ya Mungu Mwenyezi.
15 [j]"Tazama, naja kama mwizi!
Amebarikiwa yeye akeshaye na kuziweka
tayari nguo zake ili asiende uchi na
kuonekana aibu yake."
16 [k]Ndipo wakawakusanya wafalme
pamoja mahali paitwapo Armagedoni[l] kwa
Kiebrania.
17 [m]Malaika wa saba akamimina bakuli
lake angani na sauti kubwa ikatoka
mle hekaluni katika kile kiti cha enzi,
ikisema, "Imekwisha kuwa!" 18 [n]Kukawa
na mianga ya umeme wa radi, ngurumo,
radi na tetemeko kubwa la ardhi. Hapajawa
kamwe na tetemeko la ardhi kama hilo
tangu mwanadamu awepo duniani, hivyo
lilikuwa tetemeko kubwa ajabu. 19 [o]Ule mji
mkubwa ukagawanyika katika sehemu tatu,
nayo miji ya mataifa ikaanguka. Mungu
akaukumbuka Babeli Mkuu na kumpa
kikombe kilichojaa mvinyo wa ghadhabu
ya hasira yake. 20 [p]Kila kisiwa kikatoweka
wala milima haikuonekana. 21 [q]Mvua kubwa
ya mawe yenye uzito wa talanta moja[r]
ikashuka kutoka mbinguni, ikawaangukia
wanadamu. Nao wanadamu wakamlaani
Mungu kwa ajili ya hayo mapigo ya mvua
ya mawe, kwa sababu pigo hilo lilikuwa
la kutisha.

### *Kahaba Mkuu Na Mnyama*

17 [s]Mmoja wa wale malaika saba
waliokuwa na yale mabakuli saba
akaja akaniambia, "Njoo, nitakuonyesha
adhabu ya yule kahaba mkuu, aketiye juu
ya maji mengi. 2 [t]Yule ambaye wafalme

[a]**16:6** Isa 49:26
[b]**16:7** Ufu 9:6; 15:3; 19:2
[c]**16:8** Ufu 8:12; 14:18
[d]**16:9** Ufu 2:21; 11:13
[e]**16:10** Ufu 13:2; 9:2
[f]**16:11** Ufu 11:13; 2:21; 16:9, 21
[g]**16:12** Ufu 9:14; Isa 41:2
[h]**16:13** Ufu 12:3; 13:1; 19:20
[i]**16:14** 1Tim 4:1; Ufu 17:14
[j]**16:15** Lk 12:3
[k]**16:16** Ufu 9:11; Amu 5:19
[l]16 Armagedoni au Har-Magedoni ina maana Mlima Megido, mahali pa kinabii ambapo wafalme wote wa dunia watakusanyika kwa vita katika siku ya Mungu Mwenyezi.
[m]**16:17** Efe 2:2; Ufu 14:15; 11:15; 21:6
[n]**16:18** Ufu 4:5; 6:12; Dan 12:1
[o]**16:19** Ufu 17:18; 18:5; 14:8
[p]**16:20** Ufu 6:14
[q]**16:21** Eze 13:13; Kut 9:23-25
[r]21 Talanta moja ni kama kilo 34.
[s]**17:1** Ufu 15:1-7; 16:19; 19:2; Yer 51:13
[t]**17:2** Ufu 14:8; 18:3; Isa 14:8; 18:3

wa dunia walizini naye na watu wakaao
duniani walilewa kwa mvinyo wa uzinzi
wake.”
3 [a]Kisha yule malaika akanichukua
katika Roho akanipeleka jangwani. Huko
nikamwona mwanamke mmoja ameketi
juu ya mnyama mwekundu aliyejaa
majina ya kumkufuru Mungu mwili mzima.
Mnyama huyo alikuwa na vichwa saba na
pembe kumi. 4 [b]Huyo mwanamke alikuwa
amevaa mavazi ya rangi ya zambarau na
nyekundu, akimetameta kwa dhahabu,
vito vya thamani na lulu. Mkononi mwake
alikuwa ameshika kikombe cha dhahabu
kilichojaa mambo ya machukizo na uchafu
wa uzinzi wake. 5 [c]Kwenye kipaji chake cha
uso palikuwa pameandikwa jina:

“SIRI,
BABELI MKUU,
MAMA WA MAKAHABA
NA WA MACHUKIZO YA DUNIA.”

6 [d]Nikaona kuwa huyo mwanamke alikuwa
amelewa kwa damu ya watakatifu, yaani,
damu ya wale watu waliouawa kwa
ushuhuda wa Yesu.
Nilipomwona huyo mwanamke,
nilistaajabu sana. 7 [e]Ndipo yule malaika
akaniambia, “Kwa nini unastaajabu?
Nitakufafanulia siri ya huyo mwanamke
na huyo mnyama aliyempanda, mwenye
vichwa saba na pembe kumi. 8 [f]Huyo
mnyama ambaye ulimwona, wakati fulani
alikuwepo, lakini sasa hayupo, naye
atapanda kutoka lile Shimo na kwenda
kwenye maangamizo yake. Watu waishio
duniani ambao majina yao hayakuandikwa
kwenye kitabu cha uzima tangu kuumbwa
kwa ulimwengu watastaajabu kumwona
huyo mnyama, kwa maana alikuwepo
wakati fulani, na sasa hayupo, lakini
atakuwepo.
9 [g]“Hapa ndipo penye wito wa akili
pamoja na hekima. Vile vichwa saba ni
vilima saba ambavyo huyo mwanamke
amevikalia. 10 Pia hivyo vichwa saba ni
wafalme saba ambao miongoni mwao
watano wamekwisha kuanguka, yupo
mwingine hajaja bado, lakini atakapokuja,
atalazimika kukaa kwa muda mfupi. 11 [h]Yule
mnyama aliyekuwepo wakati fulani na
ambaye sasa hayupo, yeye ni mfalme wa
nane. Ni miongoni mwa wale saba, naye
anakwenda kwenye maangamizi yake.
12 [i]“Zile pembe kumi ulizoziona ni
wafalme kumi ambao bado hawajapokea
ufalme, lakini watapokea mamlaka kuwa
wafalme kwa saa moja pamoja na yule
mnyama. 13 [j]Hawa wana nia moja, nao
watamwachia yule mnyama nguvu zao
na mamlaka yao. 14 [k]Watafanya vita na
Mwana-Kondoo, lakini Mwana-Kondoo
atawashinda kwa sababu yeye ni Bwana
wa mabwana na Mfalme wa wafalme. Yeye
atakuwa pamoja na watu wake walioitwa
ambao ni wateule wake na wafuasi wake
waaminifu.”
15 [l]Kisha yule malaika akaniambia, “Yale
maji uliyoyaona yule kahaba akiwa ameketi
juu yake ni jamaa, makutano, mataifa na
lugha. 16 [m]Zile pembe kumi ulizoziona,
pamoja na huyo mnyama, watamchukia
huyo kahaba, watamfilisi na kumwacha
uchi, watamla nyama yake na kumteketeza
kwa moto. 17 [n]Kwa maana Mungu ameweka
mioyoni mwao kutimiza kusudi lake kwa
kukubali kumpa yule mnyama mamlaka
yao ya utawala mpaka maneno ya Mungu
yatakapotimia. 18 [o]Yule mwanamke
uliyemwona ni ule mji mkubwa unaotawala
juu ya wafalme wa dunia.”

[a]**17:3** Ufu 12:6-14; 13:1
[b]**17:4** Ufu 18:6, 16; Yer 51:7
[c]**17:5** Ufu 18:8
[d]**17:6** Ufu 18:24
[e]**17:7** Ufu 17:5; 17:3; 12:3
[f]**17:8** Ufu 13:10; 3:10; 13:3-8
[g]**17:9** Ufu 13:18
[h]**17:11** Ufu 17:8
[i]**17:12** Ufu 12:3; 18:10, 19
[j]**17:13** Ufu 17:17
[k]**17:14** Ufu 16:14; 19:16; 1Tim 6:15; Mt 22:14
[l]**17:15** Isa 8:7; Ufu 13:7
[m]**17:16** Ufu 18:8, 17-19; 19:18; Eze 16:37-39
[n]**17:17** Ufu 10:7
[o]**17:18** Ufu 16:19

*Kuanguka Kwa Babeli*

18 [a]Baada ya haya nikaona malaika mwingine akishuka kutoka mbinguni, akiwa na mamlaka makuu na dunia ikamulikiwa na mng'ao wake. 2 [b]Naye akalia kwa nguvu kwa sauti kubwa, akisema:

"Umeanguka! Umeanguka Babeli Mkuu!
Umekuwa makao ya mashetani
na makazi ya kila pepo mchafu,
makazi ya kila ndege na kila mnyama achukizaye.
3 [c]Kwa maana mataifa yote yamekunywa
mvinyo wa ghadhabu ya uasherati wake.
Nao wafalme wa dunia wamefanya uzinzi nao,
nao wafanyabiashara wa dunia
wametajirika kutokana na wingi wa utajiri wake."

4 [d]Kisha nikasikia sauti nyingine kutoka mbinguni ikisema:

"Tokeni katikati yake, enyi watu wangu,
ili msije mkashiriki dhambi zake,
ili msije mkapatwa na pigo lake lolote;
5 [e]kwa kuwa dhambi zake zimelundikana hadi mbinguni,
naye Mungu ameukumbuka uhalifu wake.
6 [f]Mtendee kama yeye alivyotenda;
umlipe mara mbili kwa ajili ya yale aliyotenda.
Katika kikombe chake mchanganyie
mara mbili ya kile alichochanganya.
7 [g]Mpatie mateso na huzuni nyingi sawa na
utukufu na anasa alizojipatia.
Kwa kuwa moyoni mwake hujivuna, akisema,
'Mimi ninatawala kama malkia;
mimi si mjane, wala sitaona huzuni kamwe.'
8 [h]Kwa hiyo mapigo yatampata kwa siku moja:
mauti, maombolezo na njaa.
Naye atateketezwa kwa moto,
kwa maana BWANA Mungu amhukumuye ana nguvu.

9 [i]"Wafalme wa dunia waliozini naye
na kushiriki anasa zake watakapoona
moshi wa kuungua kwake, watamlilia na
kumwombolezea. 10 [j]Kwa hofu kubwa ya
mateso yake, watasimama mbali na kulia
na wakisema:

" 'Ole! Ole, ee mji mkubwa,
ee Babeli mji wenye nguvu!
Hukumu yako imekuja katika saa moja!'

11 [k]"Wafanyabiashara wa dunia watalia
na kumwomboleza kwa sababu hakuna
anunuaye bidhaa zao tena: 12 [l]Bidhaa za
dhahabu, za fedha, za vito vya thamani
na vya lulu, kitani safi, nguo za rangi ya
zambarau, hariri, nguo nyekundu, aina zote
za miti ya udi, na vifaa vyote vya pembe za
ndovu, vifaa vyote vya miti yenye thamani
kuliko yote, shaba, chuma na marmar,
13 [m]bidhaa za mdalasini, vikolezi, za uvumba,
manemane, na uvumba wenye harufu nzuri,
za divai, na mafuta ya zeituni, za unga
mzuri na ngano; ng'ombe na kondoo; farasi
na magari; na miili na roho za wanadamu.
14 "Watasema, 'Yale matunda ambayo
roho yako iliyatamani yamekoma. Utajiri
wako wote na fahari yako vimetoweka, wala
haviwezi kupatikana tena kamwe!' 15 [n]Wale
wafanyabiashara waliotajirika kwa bidhaa
hizo kutoka kwake watasimama mbali naye

[a]**18:1** Ufu 17:1; 10:1; Eze 43:2
[b]**18:2** Ufu 18:4; Yer 51:37
[c]**18:3** Ufu 14:8; 17:2; Eze 27:9-25
[d]**18:4** Isa 48:20; 2Kor 6:17
[e]**18:5** 2Nya 28:9; Ezr 9:6; Ufu 16:19
[f]**18:6** Za 137:8; Yer 50:15-29; Ufu 14:10; 17:10
[g]**18:7** Eze 28:2-8; Za 10:6; Sef 2:15
[h]**18:8** Isa 9:14; 47:9
[i]**18:9** Ufu 14:8, 11; 19:13; Yer 51:8; Eze 26:17-18
[j]**18:10** Ufu 18:15, 17; 18:16-19; 17:12
[k]**18:11** Eze 27:27; 27:31; 18:15, 19
[l]**18:12** Eze 27:12-22
[m]**18:13** Eze 27:13; 1Tim 1:10
[n]**18:15** Ufu 18:3, 10, 17; Eze 27:31

kwa hofu kubwa ya mateso yanayompata. Watalia na kuomboleza wakipiga kelele wakisema:

16 [a]" 'Ole! Ole, ee mji mkubwa,
uliyekuwa umevikwa mavazi ya kitani safi,
ya rangi ya zambarau na nyekundu,
ukimetameta kwa dhahabu,
vito vya thamani na lulu!
17 [b]Katika muda wa saa moja utajiri wote mkubwa
kama huu umeangamia!'

"Kila nahodha, na wote wasafirio kwa meli, na wote wapatao kipato chao kutokana na bahari, watasimama mbali.
18 [c]Watakapouona moshi wa kuungua kwake watalia wakisema, 'Je, kulipata kuwako mji mkubwa kama huu?' 19 [d]Nao
watajirushia mavumbi vichwani mwao, huku wakilia na kuomboleza, wakisema:

" 'Ole! Ole, ee mji mkubwa,
mji ambao wote wenye meli baharini
walitajirika kupitia kwa mali zake!
Katika saa moja tu ameangamizwa!
20 [e]Furahia kwa ajili yake, ee mbingu!
Furahini watakatifu, mitume na manabii!
Mungu amemhukumu
kwa vile alivyowatendea ninyi.' "

21 [f]Kisha malaika mmoja mwenye nguvu akainua jiwe kubwa kama la kusagia akalitupa baharini akisema:

"Hivyo ndivyo mji mkubwa Babeli
utakavyotupwa chini kwa nguvu
wala hautaonekana tena.
22 [g]Nyimbo za wapiga vinubi na waimbaji,
wapiga filimbi na wapiga tarumbeta
kamwe hazitasikika tena ndani yako.
Ndani yako kamwe hataonekana tena fundi
mwenye ujuzi wa aina yoyote.
Wala sauti ya jiwe la kusagia
kamwe haitasikika tena.
23 [h]Mwanga wa taa
hautaangaza ndani yako tena.
Sauti ya bwana arusi na bibi arusi
kamwe haitasikika ndani yako tena.
Wafanyabiashara wako walikuwa watu maarufu wa dunia.
Mataifa yote yalipotoshwa kwa uchawi wako.
24 [i]Ndani yake ilionekana damu ya manabii na ya watakatifu
na wote waliouawa duniani."

*Shangwe Huko Mbinguni*

19 [j]Baada ya haya nikasikia sauti kama ya umati mkubwa mbinguni wakipiga kelele wakisema:

"Haleluya!
Wokovu na utukufu na uweza ni vya Mungu wetu,
2 [k]kwa maana hukumu zake
ni za kweli na za haki.
Amemhukumu yule kahaba mkuu
aliyeuharibu ulimwengu kwa uzinzi wake.
Mungu amemlipiza kisasi
kwa ajili ya damu ya watumishi wake."

3 [l]Wakasema tena kwa nguvu:

[a]**18:16** Ufu 17:4; 18:10, 19
[b]**18:17** Ufu 17:16; Eze 27:28-30
[c]**18:18** Eze 27:32; Ufu 13:4
[d]**18:19** Eze 27:30; Ufu 17:16
[e]**18:20** Yer 51:48; Ufu 12:12; 19:2
[f]**18:21** Ufu 5:2; Yer 51:63
[g]**18:22** Isa 24:8; Eze 26:13; Yer 25:10
[h]**18:23** Yer 16:9; 25:10; Isa 23:8; Nah 3:4
[i]**18:24** Ufu 16:6; 17:6; Yer 51:49
[j]**19:1** Ufu 11:15; 7:10; 4:11
[k]**19:2** Kum 32:43; Ufu 6:10
[l]**19:3** Isa 34:10; Ufu 14:11

"Haleluya!
Moshi wake huyo kahaba unapanda juu
milele na milele."

4 [a]Wale wazee ishirini na wanne pamoja na wale viumbe wanne wenye uhai wakaanguka kifudifudi, wakamwabudu Mungu, aliyekuwa ameketi kwenye kile kiti cha enzi. Wakasema kwa sauti kuu:

"Amen, Haleluya!"

5 [b]Kisha sauti ikatoka katika kile kiti cha enzi, ikisema:

"Msifuni Mungu wetu,
ninyi watumishi wake wote,
ninyi nyote mnaomcha,
wadogo kwa wakubwa!"

6 [c]Kisha nikasikia sauti kama ya umati mkubwa, kama sauti ya maji mengi yaendayo kasi na kama ngurumo kubwa ya radi wakipiga kelele wakisema:

"Haleluya!
Kwa maana Bwana Mungu wetu
Mwenyezi anatawala.
7 [d]Tufurahi, tushangilie
na kumpa utukufu!
Kwa maana arusi ya Mwana-Kondoo imewadia
na bibi arusi wake amejiweka tayari.
8 [e]Akapewa kitani safi, nyeupe
inayong'aa, ili avae."

(Hiyo kitani safi inawakilisha matendo ya haki ya watakatifu.)

9 [f]Ndipo malaika akaniambia, "Andika: 'Wamebarikiwa wale walioalikwa kwenye karamu ya arusi ya Mwana-Kondoo!' " Naye akaongeza kusema, "Haya ndiyo maneno ya kweli ya Mungu."

10 [g]Ndipo nikaanguka kifudifudi miguuni pake ili kumwabudu, lakini yeye akaniambia, "Usifanye hivyo! Mimi pia ni mtumishi mwenzako pamoja na ndugu zako walio na ushuhuda wa Yesu. Mwabudu Mungu! Maana ushuhuda wa Yesu ndio roho ya unabii."

### *Aliyepanda Farasi Mweupe*

11 [h]Kisha nikaona mbingu imefunguka na hapo mbele yangu akiwepo farasi mweupe, ambaye yeye aliyempanda aliitwa Mwaminifu na Kweli. Yeye huhukumu kwa haki na kufanya vita.
12 [i]Macho yake ni kama miali ya moto na juu ya kichwa chake kuna taji nyingi. Ana jina lililoandikwa ambalo hakuna mtu yeyote anayelijua isipokuwa yeye mwenyewe.
13 [j]Amevaa joho lililochoviwa katika damu, na Jina lake ni "Neno la Mungu."
14 [k]Majeshi ya mbinguni walikuwa wakimfuata, wakiwa wamepanda farasi weupe, hali wamevaa mavazi ya kitani safi, nyeupe na nzuri.
15 [l]Kinywani mwake hutoka upanga mkali ambao kwa huo atayaangusha mataifa. "Atayatawala kwa fimbo yake ya utawala ya chuma." Hulikanyaga shinikizo la mvinyo wa ghadhabu ya Mungu Mwenyezi.
16 [m]Kwenye joho lake na paja lake pameandikwa jina hili:

MFALME WA WAFALME, NA BWANA WA MABWANA.

### *Mnyama Na Majeshi Yake Yashindwa*

17 [n]Nami nikamwona malaika amesimama ndani kwenye jua, akaita ndege wote warukao angani kwa sauti kuu, "Njooni, kusanyikeni kwa ajili ya karamu kubwa ya Mungu,
18 [o]ili mpate kula nyama ya wafalme

[a]**19:4** Ufu 4:4-6; 5:14
[b]**19:5** Za 134:1; Ufu 11:18
[c]**19:6** Ufu 11:15
[d]**19:7** Mt 25:10; Efe 5:32; Ufu 21:2, 9
[e]**19:8** Ufu 15:4; 19:14; 15:6; Isa 61:10; Eze 44:17; Zek 3:4
[f]**19:9** Ufu 1:19; Lk 14:15; Ufu 21:5; 22:6
[g]**19:10** Ufu 22:8; Mdo 10:25, 26; Ufu 22:9; 12:17
[h]**19:11** Ufu 6:2; 3:14; Kut 15:3
[i]**19:12** Ufu 1:14; 6:2; 2:17
[j]**19:13** Isa 63:2, 3; Yn 1:1
[k]**19:14** Ufu 19:8; 3:4; 17:14
[l]**19:15** Ufu 1:16; 12:5; 14:20; Isa 11:4; 2The 2:8; Za 2:9
[m]**19:16** Ufu 17:14; 19:12; 1Tim 6:15
[n]**19:17** Ufu 8:13; Eze 39:17
[o]**19:18** Eze 39:18-20

na ya majemadari, ya mashujaa, ya farasi
na ya wapanda farasi, nyama ya wanadamu,
wote walio huru na watumwa, wadogo na
wakubwa."
19 [a]Kisha nikamwona yule mnyama na
wafalme wa dunia pamoja na majeshi
yao wakiwa wamekusanyika pamoja ili
kufanya vita dhidi ya yule aliyempanda
farasi pamoja na jeshi lake. 20 [b]Lakini yule
mnyama akakamatwa pamoja na huyo nabii
wa uongo ambaye alikuwa amefanya ishara
kwa niaba ya huyo mnyama, ambaye kwa
ishara hizi aliwadanganya wale waliopokea
chapa ya huyo mnyama na kuiabudu
sanamu yake. Hawa wawili wakatupwa
wakiwa hai ndani ya ziwa la moto liwakalo
kwa kiberiti. 21 Wale waliosalia waliuawa
kwa upanga uliotoka kinywani mwa yule
aliyekuwa amempanda farasi nao ndege
wote wakajishibisha kwa nyama yao.

*Utawala Wa Miaka Elfu Moja*

20 [c]Kisha nikaona malaika akishuka
kutoka mbinguni, akiwa ameshika
ufunguo wa lile Shimo na mnyororo
mkubwa mkononi mwake. 2 [d]Akalishika lile
joka, yule nyoka wa zamani, ambaye ndiye
ibilisi au Shetani, naye akamfunga kwa
muda wa miaka 1,000. 3 [e]Akamtupa katika
lile Shimo, akamfunga humo na kulitia
lakiri, ili kumzuia asiendelee kudanganya
mataifa mpaka hiyo miaka 1,000 itimie.
Baada ya hayo lazima afunguliwe kwa
muda mfupi.
4 [f]Kisha nikaona viti vya enzi vilivyokuwa
vimekaliwa na hao waliopewa mamlaka
ya kuhukumu, na nikaona roho za wale
waliokatwa vichwa kwa sababu ya ushuhuda
wa Yesu na kwa sababu ya neno la Mungu.
Hawakuwa wamemsujudu huyo mnyama
wala sanamu yake wala hawakupokea ile
chapa yake kwenye vipaji vya nyuso zao
au kwenye mikono yao. Wakawa hai na
kutawala pamoja na Kristo miaka 1,000.
5 [g](Wafu waliosalia hawakufufuka mpaka
ilipotimia hiyo miaka 1,000.) Huu ndio
ufufuo wa kwanza. 6 [h]Waliobarikiwa na
walio watakatifu ni wale walio na sehemu
katika ufufuo wa kwanza. Hao mauti ya
pili haina nguvu juu yao, bali watakuwa
makuhani wa Mungu na wa Kristo, nao
watatawala pamoja naye kwa muda wa
miaka 1,000.

*Kuhukumiwa Kwa Shetani*

7 [i]Hiyo miaka 1,000 itakapotimia,
Shetani atafunguliwa kutoka kifungoni
mwake, 8 [j]naye atatoka ili kuyadanganya
mataifa yaliyopo katika pembe nne za
dunia, yaani, Gogu na Magogu apate
kuwakusanya tayari kwa vita. Idadi yao
ni kama mchanga ulioko pwani. 9 [k]Nao
walitembea katika eneo lote la dunia,
wakaizunguka kambi ya watakatifu na ule
mji unaopendwa. Lakini moto ukashuka
kutoka mbinguni na kuwateketeza. 10 [l]Naye
ibilisi aliyewadanganya akatupwa katika
ziwa la moto na kiberiti walikokuwa
wametupwa yule mnyama na yule nabii wa
uongo. Watateswa humo usiku na mchana,
milele na milele.

*Wafu Wanahukumiwa*

11 [m]Kisha nikaona kiti kikubwa cheupe
cha enzi pamoja na yeye aliyeketi juu yake.
Dunia na mbingu zikaukimbia uso wake
wala mahali pao hapakuonekana. 12 [n]Nami
nikawaona wafu wakubwa na wadogo,
wakiwa wamesimama mbele ya hicho kiti
cha enzi na vitabu vikafunguliwa. Pia kitabu
kingine kikafunguliwa ambacho ni kitabu
cha uzima. Hao wafu wakahukumiwa
sawasawa na matendo yao kama
yalivyoandikwa ndani ya hivyo vitabu.

---

[a]**19:19** Ufu 16:14, 16
[b]**19:20** Ufu 16:13; 13:12; Dan 7:11; Ufu 21:8; 14:19
[c]**20:1** Ufu 10:1; 1:18
[d]**20:2** Ufu 12:9; 2Pet 2:4
[e]**20:3** Dan 6:17; Ufu 12:9
[f]**20:4** Dan 7:9; Ufu 6:9; 13:12, 16
[g]**20:5** Lk 14:14; 1The 4:16
[h]**20:6** Ufu 14:13; 2:11; 1:6
[i]**20:7** Ufu 20:2
[j]**20:8** Eze 38:2; 39:1; Ufu 1:6
[k]**20:9** Eze 38:9, 16; 39:6; Za 87:2; Ufu 13:13
[l]**20:10** Ufu 19:20; 14:10, 11; Za 2:9
[m]**20:11** Ufu 4:2; 6:14; Mt 25:31-46; Dan 2:35
[n]**20:12** Dan 7:10; Mal 3:16; Yer 17:10; Mt 16:27

13 [a]Bahari ikawatoa wafu waliokuwamo
ndani yake, nayo mauti na Kuzimu
zikawatoa wafu waliokuwamo ndani yake.
Kila mtu akahukumiwa kulingana na yale
aliyoyatenda. 14 [b]Kisha mauti na Kuzimu
zikatupwa katika ziwa la moto. Hii ndio
mauti ya pili, yaani, hilo ziwa la moto.
15 [c]Iwapo mtu jina lake halikuonekana
katika kile kitabu cha uzima, alitupwa
ndani ya lile ziwa la moto.

*Mbingu Mpya Na Nchi Mpya*

21 [d]Kisha nikaona mbingu mpya na nchi
mpya, kwa maana mbingu za kwanza
na nchi ya kwanza vimekwisha kupita, wala
hapakuwepo na bahari tena. 2 [e]Nikaona Mji
Mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka
kutoka mbinguni kwa Mungu, ukiwa
umeandaliwa kama bibi arusi aliyepambwa
kwa ajili ya mumewe. 3 [f]Nami nikasikia
sauti kubwa kutoka kile kiti cha enzi
ikisema, “Sasa makao ya Mungu ni pamoja
na wanadamu, naye atakaa pamoja nao.
Yeye atakuwa Mungu wao nao watakuwa
watu wake, naye Mungu mwenyewe
atakuwa pamoja nao. 4 [g]Atafuta kila chozi
kutoka macho yao. Mauti haitakuwepo
tena, wala maombolezo, wala kilio, wala
maumivu, kwa maana mambo ya kwanza
yamekwisha kupita.”
5 [h]Naye yule aliyeketi juu ya kile kiti cha
enzi akasema, “Tazama, nayafanya mambo
yote kuwa mapya!” Kisha akasema, “Andika
haya, maana maneno haya ni ya kuaminika
tena ni kweli.”
6 [i]Akaniambia, “Imekwisha kuwa. Mimi
ni Alfa na Omega, Mwanzo na Mwisho.
Yeye aonaye kiu nitampa kunywa kutoka
chemchemi ya maji ya uzima bila gharama
yoyote. 7 [j]Yeye ashindaye atayarithi haya
yote, nami nitakuwa Mungu wake, naye
atakuwa mwanangu. 8 [k]Lakini waoga,
wasioamini, wachafu, wauaji, wazinzi,
wachawi, waabudu sanamu, pamoja na
waongo wote, mahali pao ni katika lile
ziwa liwakalo moto na kiberiti. Hii ndiyo
mauti ya pili.”
9 [l]Mmoja wa wale malaika saba
waliokuwa na yale mabakuli saba ya hayo
mapigo saba ya mwisho akaja akaniambia,
“Njoo, nami nitakuonyesha bibi arusi,
yaani, mke wa Mwana-Kondoo.” 10 [m]Naye
akanichukua katika Roho hadi kwenye
mlima mkubwa na mrefu, akanionyesha
ule Mji Mtakatifu, Yerusalemu, ukishuka
kutoka mbinguni kwa Mungu. 11 [n]Ulikuwa
uking’aa kwa utukufu wa Mungu kama
kito chenye thamani sana, kama yaspi,
safi kama kioo. 12 [o]Ulikuwa na ukuta
mkubwa, mrefu wenye malango kumi na
mawili, pakiwa na malaika kumi na wawili
kwenye hayo malango. Kwenye malango
hayo yaliandikwa majina ya yale makabila
kumi na mawili ya Israeli. 13 [p]Kulikuwa na
malango matatu upande wa mashariki,
matatu upande wa kaskazini, matatu
upande wa kusini na matatu upande wa
magharibi. 14 [qr]Ukuta wa huo mji ulikuwa
na misingi kumi na miwili, na juu yake
yaliandikwa majina ya wale mitume kumi
na wawili wa Mwana-Kondoo.
15 Huyo malaika aliyesema nami alikuwa
na ufito wa dhahabu wa kupimia huo mji,
malango yake na kuta zake. 16 [s]Mji huo
ulikuwa mraba, urefu wake ulikuwa sawa
na upana wake. Akaupima huo mji kwa huo
ufito akakuta una kama kilomita 2,200;[t]
urefu wake na upana wake na kwenda juu

[a]**20:13** Ufu 6:8; Isa 26:19
[b]**20:14** 1Kor 15:26; Ufu 20:13; 19:20; 2:11
[c]**20:15** Dan 12:1; Mt 25:41
[d]**21:1** Isa 65:17; 2Pet 3:13
[e]**21:2** Ebr 11:10; 12:22
[f]**21:3** 2Kor 6:16; Zek 2:10; Isa 8:8
[g]**21:4** Ufu 7:17; 1Kor 15:26; Isa 35:10; 65:19
[h]**21:5** Ufu 4:9; 20:11; 19:9
[i]**21:6** Ufu 16:17; 1:8; 22:13; Yn 4:10
[j]**21:7** Ufu 2:7; 2Sam 7:14
[k]**21:8** Za 5:6; Ufu 2:11
[l]**21:9** Ufu 15:1, 6, 7; 19:7
[m]**21:10** Ufu 17:3; 1:10; Eze 40:2; Ufu 21:2
[n]**21:11** Ufu 15:8; 4:6; Isa 60:1, 2; Eze 43:2; Ufu 21:23; 21:18, 19
[o]**21:12** Eze 48:30-34
[p]**21:13** Eze 48:31, 34
[q]**21:14** Efe 2:20; Ebr 11:10; Mdo 1:26
[r]**21:14** Ufu 11:1; Eze 40:3; Ufu 21:12
[s]**21:16** Eze 45:16; 48:16; 17
[t]16 Kilomita 2,200 hapa ni sawa na maili 1,200.

kwake vilikuwa sawa. 17 [a]Akaupima ukuta
wake, ulikuwa na unene wa dhiraa 144[b]
kwa kipimo cha kibinadamu ambacho huyo
malaika alikuwa akikitumia. 18 [c]Ukuta huo
ulijengwa kwa yaspi hali mji wenyewe
ulijengwa kwa dhahabu safi, iking'aa
kama kioo. 19 [d]Misingi ya kuta za mji huo
zilipambwa kwa kila aina ya kito cha
thamani. Msingi wa kwanza ulikuwa wa
yaspi, wa pili yakuti samawi, wa tatu
kalkedoni, wa nne zumaridi, 20 [e]wa tano
sardoniki, wa sita akiki, wa saba krisolitho,
wa nane zabarajadi, wa tisa yakuti manjano,
wa kumi krisopraso, wa kumi na moja
hiakintho, wa kumi na mbili amethisto.
21 [f]Yale malango kumi na mbili yalikuwa
ni lulu kumi na mbili, kila lango lilikuwa
limetengenezwa kwa lulu moja. Barabara
kuu ya mji huo ilikuwa ya dhahabu safi
ing'aayo kama kioo.

22 [g]Sikuona Hekalu ndani ya huo mji
kwa sababu Bwana Mungu Mwenyezi na
Mwana-Kondoo ndio hekalu lake. 23 [h]Ule mji
hauhitaji jua wala mwezi kuuangazia, kwa
sababu utukufu wa Mungu ndio nuru yake na
Mwana-Kondoo ndiye taa yake. 24 [i]Mataifa
yatatembea yakiangaziwa na nuru yake na
wafalme wa duniani wataleta fahari yao
ndani yake. 25 [j]Malango yake hayatafungwa
kamwe, kwa maana hakutakuwa na usiku
humo. 26 [k]Utukufu na heshima za mataifa
zitaletwa humo. 27 [l]Lakini kitu kichafu
hakitaingia humo kamwe, wala mtu yeyote
atendaye mambo ya aibu au ya udanganyifu.
Bali watakaoingia humo ni wale tu ambao
majina yao yameandikwa katika kitabu cha
uzima cha Mwana-Kondoo.

---

[a]**21:17** Ufu 13:18
[b]17 Dhiraa 144 ni karibu mita 65.
[c]**21:18** Ufu 21:11, 21
[d]**21:19** Kut 28:17-20
[e]**21:20** Ufu 4:3
[f]**21:21** Ufu 21:12; Isa 54:12; Ufu 21:18
[g]**21:22** Yn 4:21-23; Ufu 1:8; 5:6
[h]**21:23** Isa 24:23; 22:5
[i]**21:24** Isa 60:3, 5
[j]**21:25** Isa 60:11; Zek 14:7; Ufu 22:5
[k]**21:26** Ufu 21:24
[l]**21:27** Yoe 3:17; Ufu 22:14, 15

### *Mto Wa Maji Ya Uzima*

22 [m]Kisha yule malaika akanionyesha mto
wa maji ya uzima, maangavu kama
kioo yakitiririka kutoka kwenye kile kiti
cha enzi cha Mungu na cha Mwana-Kondoo,
2 [n]kupitia katikati ya barabara kuu ya huo
mji. Kwenye kila upande wa huo mto
kulikuwa na mti wa uzima utoao matunda
ya aina kumi na mbili, ukizaa matunda
yake kila mwezi. Nayo majani ya mti huo ni
kwa ajili ya uponyaji wa mataifa. 3 [o]Katika
mji huo hakutakuwa tena na laana, bali
kiti cha enzi cha Mungu na cha Mwana-
Kondoo kitakuwamo humo na watumishi
wake watamtumikia, 4 [p]nao watamwona uso
wake na Jina lake litakuwa kwenye vipaji
vya nyuso zao. 5 [q]Usiku hautakuwako tena,
wala hawatahitaji mwanga wa taa au wa
jua, kwa maana Bwana Mungu atakuwa
nuru yao, nao watatawala milele na milele.

6 [r]Kisha yule malaika akaniambia,
"Maneno haya ni ya kuaminika na kweli.
Bwana, Mungu wa roho za manabii,
alimtuma malaika wake kuwaonyesha
watumishi wake yale ambayo hayana budi
kutukia upesi."

### *Bwana Yesu Anakuja*

7 [s]"Tazama, naja upesi! Amebarikiwa
yeye ayashikaye maneno ya unabii wa
kitabu hiki."

8 [t]Mimi, Yohana, ndiye niliyesikia na
kuyaona mambo haya. Nami nilipokwisha
kuyasikia na kuyaona, nilianguka chini
nikasujudu miguuni pa yule malaika
aliyekuwa akinionyesha mambo hayo.
9 [u]Lakini yeye akaniambia, "Usifanye
hivyo! Mimi ni mtumishi pamoja nawe na
ndugu zako manabii na wote wanaoyashika
maneno ya kitabu hiki. Msujudie Mungu!"

---

[m]**22:1** Ufu 4:6; Eze 47:1; Zek 14:8
[n]**22:2** Ufu 2:7; Eze 47:12
[o]**22:3** Zek 14:11; Ufu 7:15
[p]**22:4** Mt 5:8; Ufu 14:1
[q]**22:5** Ufu 21:23, 25; 20:4; Dan 7:27
[r]**22:6** Ufu 1:1; 19:9; 21:5; Ebr 12:9
[s]**22:7** Ufu 3:11; 1:3; Mt 16:27; Ufu 22:10, 18, 19
[t]**22:8** Ufu 1:1; 19:10
[u]**22:9** Ufu 19:10; 22:10, 18, 19

10 [a]Kisha akaniambia, “Usiyafunge
maneno ya unabii yaliyomo katika kitabu
hiki, kwa sababu wakati umekaribia.
11 [b]Atendaye mabaya na aendelee kutenda
mabaya, aliye mchafu na aendelee kuwa
mchafu, yeye atendaye haki na aendelee
kutenda haki, na yeye aliye mtakatifu na
aendelee kuwa mtakatifu.”

12 [c]“Tazama, naja upesi! Thawabu yangu
i mkononi mwangu, nami nitampa kila mtu
sawasawa na alivyotenda. 13 [d]Mimi ni Alfa
na Omega, wa Kwanza na wa Mwisho,
Mwanzo na Mwisho.

14 [e]“Wamebarikiwa wale wafuao mavazi
yao, ili wapate haki ya kuuendea huo mti
wa uzima na kuuingia huo mji kupitia
kwenye malango yake. 15 [f]Huko nje wako
mbwa, wachawi, wazinzi, wauaji, waabudu
sanamu, na kila mtu apendaye udanganyifu
na kuufanya.

16 [g]“Mimi, Yesu, nimemtuma malaika
wangu kushuhudia mambo haya kwa ajili
ya makanisa. Mimi ndimi Shina na Mzao
wa Daudi, ile Nyota ya Asubuhi ing’aayo.”

17 [h]Roho na bibi arusi wanasema, “Njoo!”
Naye asikiaye na aseme, “Njoo!” Yeyote
mwenye kiu na aje, na kila anayetaka na
anywe maji ya uzima bure.

18 [i]Namwonya kila mtu asikiaye
maneno ya unabii wa kitabu hiki: Mtu
yeyote akiongeza humo chochote, Mungu
atamwongezea mapigo yaliyoandikwa
katika kitabu hiki. 19 [j]Kama mtu yeyote
akipunguza humo chochote katika
maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mungu
atamwondolea sehemu yake katika ule
mti wa uzima na katika ule mji mtakatifu,
ambao habari zake zimeandikwa katika
kitabu hiki.

20 [k]Yeye anayeshuhudia mambo haya
asema, “Hakika, naja upesi!”

Amen. Njoo, Bwana Yesu.

21 [l]Neema ya Bwana Yesu iwe na
watakatifu wote. Amen.

---

[a]**22:10** Dan 8:26; Ufu 10:4; 1:3
[b]**22:11** Eze 3:27; Dan 12:10
[c]**22:12** Isa 14:10; Mt 16:27; Isa 62:11
[d]**22:13** Ufu 1:8, 17; 21:6
[e]**22:14** Ufu 2:7; 21:12, 27
[f]**22:15** Kum 23:18; Kol 3:5, 6; Flp 3:2
[g]**22:16** Ufu 1:1, 4; 5:5; 2Pet 1:19; Ufu 2:28
[h]**22:17** Ufu 14:13
[i]**22:18** Kum 12:32; Mit 30:6; Ufu 5:6; 16:21
[j]**22:19** Kum 4:2
[k]**22:20** Ufu 1:2; 1Kor 16:22
[l]**22:21** Rum 16:20